

BIBLIA TAKATIFU

— TAFSIRI YA ULIMWENGU MPYA —

Biblia hii ni ya

BIBLIA TAKATIFU

— TAFSIRI YA ULIMWENGU MPYA —

Biblia hii imetafsiriwa kutokana na tafsiri ya
Kiingereza ya *New World Translation* (Toleo la 2013).

Imetafsiriwa kwa kutegemea lugha za awali
zilizotumiwa kuandika Biblia

**“BWANA MWENYE ENZI KUU YEHOVA
[יהוה, YHWH] ANASEMA HIVI: ‘ . . . TAZAMA! NINAUMBA
MBINGU MPYA NA DUNIA MPYA; NA MAMBO YA ZAMANI HAYATA-
INGIA TENA AKILINI, WALA HAYATAINGIA TENA MOYONI.’ ”**

—Isaya 65:13, 17; tazama pia 2 Petro 3:13.

© 2017

WATCH TOWER BIBLE
AND TRACT SOCIETY
OF PENNSYLVANIA

200 Watchtower Drive
Patterson, NY 12563-9205
U.S.A.

WACHAPISHAJI

WATCHTOWER BIBLE AND
TRACT SOCIETY OF NEW
YORK, INC.

Wallkill, New York, U.S.A.

Biblia hii imechapishwa ikiwa
nzima au kwa sehemu katika
lugha zaidi ya 240. Unaweza
kupata orodha kamili ya lu-
gha kwenye tovuti ya
www.jw.org/sw.

Jumla ya Nakala Zilizocha-
pishwa za Matoleo Yote ya
Tafsiri ya Ulimwengu Mpya:

Nakala 244,746,446

Chapa ya 2023

Biblia hii haiuzwi. Ni sehemu
ya kazi ya elimu ya Biblia ya
ulimwenguni pote inayofa-
nywa na Mashahidi wa
Yehova.

Biblia Takatifu

—*Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*

*New World Translation of the
Holy Scriptures*

Swahili (*nwt-SW*)

Made in Japan

Imechapishiwa Japani

4-7-1 Nakashinden,
Ebina City, Kanagawa-Pref,
243-0496
Japan

Photo Credits:

Page 2048:

Top: Courtesy of Shrine of
the Book, The Israel Museum,
Jerusalem

Bottom: Courtesy of Ben-Zvi
Institute; photographer:
Ardon Bar-Hama

Page 2050:

© The Trustees of the
Chester Beatty Library,
Dublin

Page 2052:

Shrine of the Book,
Photo © The Israel Museum,
Jerusalem

Page 2054:

© The British Library Board
(G.12161)

Page 2058:

Left: From the book
*A Pre-Massoretic Biblical
Papyrus*, by Stanley A. Cook,
M. A. (1903)

Page 2059:

From *The Codex Alexandrinus
in Reduced Photographic
Facsimile*, 1909



Utangulizi wa Neno la Mungu

Biblia ina ujumbe wa Mungu kwa ajili yetu leo. Inatuonyesha jinsi ya kuishi kwa mafanikio na jinsi ya kupata kibali cha Mungu. Pia, inajibu maswali yafuatayo:

1. Mungu ni nani?	12. Kuna tumaini gani kwa ajili ya wafu?
2. Unawezaje kujifunza kumhusu Mungu?	13. Biblia inasema nini kuhusu kufanya kazi?
3. Ni nani aliyeandika Biblia?	14. Unawezaje kutumia vizuri pesa na mali zako?
4. Je, Biblia ni sahihi kisayansi?	15. Unawezaje kuwa na furaha?
5. Biblia ina ujumbe gani?	16. Unawezaje kukabiliana na mahangaiko?
6. Biblia ilitabiri nini kumhusu Masihi?	17. Biblia inawezaje kuisaidia familia yako?
7. Biblia ilitabiri nini kuhusu nyakati zetu?	18. Unawezaje kumkaribia Mungu?
8. Je, Mungu ndiye chanzo cha mateso yanayotupata?	19. Vitabu vya Biblia vina ujumbe gani?
9. Kwa nini wanadamu huteseka?	20. Unawezaje kunufaika zaidi unaposoma Biblia?
10. Biblia inaahidi nini kuhusu wakati ujao?	
11. Ni nini hutokea mtu anapokufa?	

JINSI YA KUPATA MISTARI YA BIBLIA

Biblia ina vitabu vidogo 66. Imegawanywa katika sehemu mbili: Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu (“Agano la Kale”) na Maandiko ya Kigiriki (“Agano Jipya”). Kila kitabu cha Biblia kimegawanywa kwa sura na mistari. Maandiko yanapotajwa, nambari ya kwanza baada ya jina la kitabu inaonyesha sura, na nambari inayofuata au zinazofuata ni mstari au mistari. Kwa mfano, Mwanzo 1:1 inamaanisha Mwanzo sura ya 1, mstari wa 1.

Mungu ni nani?

“Na watu wajue kwamba wewe, ambaye jina lako ni Yehova, wewe peke yako ndiye Uliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote.”

Zaburi 83:18 [Ukurasa wa 977]

“Jueni kwamba Yehova ni Mungu. Yeye ndiye aliyetuu- mba, na sisi ni mali yake.”

Zaburi 100:3 [Ukurasa wa 991]

“Mimi ni Yehova. Hilo ndilo jina langu; simpi yeyote utukufu wangu, wala kuzipa sanamu za kuchongwa sifa yangu.”

Isaya 42:8 [Ukurasa wa 1185]

“Kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokolewa.”

Waroma 10:13 [Ukurasa wa 1810]

“Bila shaka, kila nyumba hujengwa na mtu fulani, lakini yule aliyevijenga vitu vyote ni Mungu.”

Waebrania 3:4 [Ukurasa wa 1912]

“Inueni macho yenu mbinguni mwone. Ni nani aliye-
viumba vitu hivi? Ni Yule anayelileta nje jeshi lao kwa
hesabu; huziita zote kwa majina. Kwa sababu ya nguvu
zake nyingi zenye msukumo na nguvu zake zenye kuo-
gopesha, hakuna hata moja inayokosekana.”

Isaya 40:26 [Ukurasa wa 1182]



Unawezaje kujifunza kumhusu Mungu?

“Kitabu hiki cha Sheria kisiondoke kinywani mwako, ni lazima ukisome kwa sauti ya chini mchana na usiku ili ufuata kwa uangalifu mambo yote yaliyoandikwa humo; ndipo utakapofanikisha njia yako na kutenda kwa hekima.”

Yoshua 1:8 [Ukurasa wa 382]

“Wakaendelea kusoma kwa sauti kubwa kitabu hicho cha Sheria ya Mungu wa kweli, nao wakafafanua, na kueleza maana yake; hivyo wakawasaidia watu kuelewa mambo yaliyokuwa yakisomwa.”

Nehemia 8:8 [Ukurasa wa 805]

“Mwenye furaha ni mtu ambaye hatembezi katika mashauri ya waovu . . . , lakini anapendezwa na sheria ya Yehova, naye huisoma sheria Yake kwa sauti ya chini mchana na usiku. . . . Kila jambo analofanya litafanikiwa.”

Zaburi 1:1-3 [Ukurasa wa 897]

“Filipo akakimbia kandokando na kumsikia akimsoma kwa sauti kubwa nabii Isaya, akamuuliza: ‘Je, kweli unajua unayosoma?’ Akajibu: ‘Kwa kweli, ninawezaje kuyaelewa mtu fulani asiponiongoza?’”

Matendo 8:30, 31 [Ukurasa wa 1756]

“Sifa zake zisizoonekana, zinaonekana waziwazi tangu kuumbwa kwa ulimwengu na kuendelea, kwa sababu zinaeleweka kupitia vitu vilivyoundwa, yaani, nguvu zake za milele na Uungu, hivi kwamba hawana sababu ya kujitetea.”

Waroma 1:20 [Ukurasa wa 1797]

“Tafakari mambo haya; zama katika hayo, ili maendeleo yako yaonekane wazi kwa watu wote.”

1 Timotheo 4:15 [Ukurasa wa 1897]

“Acheni tufikiriane ili kuchocheana katika upendo na matendo mazuri, bila kuacha kukutana pamoja.”

Waebrania 10:24, 25 [Ukurasa wa 1921]

“Ikiwa yeyote kati yenu anakosa hekima, na aendeleo kumwomba Mungu, kwa maana yeye huwapa wote kwa ukarimu na bila kushutumu, naye atapewa.”

Yakobo 1:5 [Ukurasa wa 1928]

Ni nani aliyeandika Biblia?

“Musa akaandika maneno yote ya Yehova.”

Kutoka 24:4 [Ukurasa wa 166]

“Danieli aliota ndoto na kuona maono akiwa amelala kitandani mwake. Kisha akaandika ndoto hiyo; akaandika masimulizi kamili ya mambo hayo.”

Danieli 7:1 [Ukurasa wa 1452]

“Mlipolipokea neno la Mungu, ambalo mlilisikia kutoka kwetu, mlilikubali si kama neno la wanadamu, bali kama lilivyo kwa kweli, kama neno la Mungu.”

1 Wathesalonike 2:13 [Ukurasa wa 1887]

“Kila Andiko limeongozwa na roho ya Mungu nalo ni lenye faida kwa kufundisha.”

2 Timotheo 3:16 [Ukurasa wa 1904]

“Unabii haukuletwa wakati wowote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walisema yaliyotoka kwa Mungu kama walivyoongozwa na roho takatifu.”

2 Petro 1:21 [Ukurasa wa 1942]

Je, Biblia ni sahihi kisayansi?

“Hulitandaza anga la kaskazini mahali pasipo na kitu, na kuining’iniza dunia mahali pasipo na kitu.”

Ayubu 26:7 [Ukurasa wa 864]

“Vijito vyote hutiririka kuingia baharini, lakini bado bahari haijai. Mahali vijito vinakotoka, huko ndiko vinakorudi ili vitiririke tena.”

Mhubiri 1:7 [Ukurasa wa 1093]

“Kuna Yule anayekaa juu ya duara ya dunia.”

Isaya 40:22 [Ukurasa wa 1181]



Biblia ina ujumbe gani?

“Nitaweka uadui kati yako na mwanamke na kati ya uzao wako na uzao wake. Yeye atakuponda kichwa, nawe utamuuma kisigino.”

Mwanzo 3:15 [Ukurasa wa 47]

“Kupitia uzao wako mataifa yote ya dunia yatajipatia baraka kwa sababu umeisikiliza sauti yangu.”

Mwanzo 22:18 [Ukurasa wa 73]

“Ufalme wako na uje. Mapenzi yako na yatendeke duniani kama pia ilivyo mbinguni.”

Mathayo 6:10 [Ukurasa wa 1565]

“Kwa upande wake, Mungu anayetoa amani atamponda Shetani chini ya miguu yenu hivi karibuni.”

Waroma 16:20 [Ukurasa wa 1818]

“Vitu vyote vitakapotiishwa kwake, ndipo Mwana mweyewe atakapojitiisha pia kwa Yule aliyevitiisha vitu vyote kwake, ili Mungu awe vitu vyote kwa kila mtu.”

1 Wakorintho 15:28 [Ukurasa wa 1839]

“Sasa ahadi zilitolewa kwa Abrahamu na kwa uzao wake . . . , ambaye ni Kristo. Isitoshe, ikiwa ninyi ni wa Kristo, ninyi kwa kweli ni uzao wa Abrahamu.”

Wagalatia 3:16, 29 [Ukurasa wa 1861, 1862]

“Ufalme wa ulimwengu umekuwa Ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala akiwa mfalme milele na milele.”

Ufunuo 11:15 [Ukurasa wa 1969]

“Basi yule joka mkubwa akatupwa chini, yule nyoka wa zamani, anayeitwa Ibilisi na Shetani, anayeipotosha dunia nzima inayokaliwa; akatupwa chini duniani, na malaika zake wakatupwa chini pamoja naye.”

Ufunuo 12:9 [Ukurasa wa 1970]

“Akamkamata yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, na kumfunga kwa miaka 1,000.”

Ufunuo 20:2 [Ukurasa wa 1979]

Biblia ilitabiri nini kumhusu Masihi?

UNABII

“Wewe, Ee Bethlehemu Efratha, . . . kutoka kwa-ko atatoka kwa ajili yangu yule atakayekuwa mtawala katika Israeli.”

Mika 5:2 [Ukurasa wa 1512]

UTIMIZO

“Baada ya Yesu kuzaliwa huko Bethlehemu ya Yudea katika siku za Mfalme Herode, tazama! wanajimu kutoka Mashariki walikuja Yerusalemu.”

Mathayo 2:1 [Ukurasa wa 1559]

“Wanagawana mavazi yangu, nao wanalipigia kura vazi langu.”

Zaburi 22:18 [Ukurasa wa 914]

“Baada ya wanajeshi kumtundika Yesu kwenye mti, wakachukua mavazi yake ya nje na kuyagawanya vipande vinne . . . Lakini vazi la ndani hali-kuwa na mshono, lilikuwa limefumwa kutoka juu mpaka chini. Basi wakaa- mbiana: ‘Tusilirarue, badala yake tupige kura ili tuamue litakuwa la nani.’”

Yohana 19:23, 24

[Ukurasa wa 1735]

UNABII

“Anailinda mifupa yake yote; Haujavunjwa hata mmoja.”

Zaburi 34:20 [Ukurasa wa 926]

UTIMIZO

“Walipomfikia Yesu, waliona kwamba tayari amekufa, kwa hiyo hawakuivunja miguu yake.”

Yohana 19:33 [Ukurasa wa 1735]

“Alichomwa kwa sababu ya makosa yetu.”

Isaya 53:5 [Ukurasa wa 1206]

“Mwanajeshi mmoja akauchoma ubavu wa Yesu kwa mkuki, na mara moja damu na maji vikatoka.”

Yohana 19:34 [Ukurasa wa 1735]

“Wakanilipa mshahara wangu, vipande 30 vya fedha.”

Zekaria 11:12, 13
[Ukurasa wa 1546]

“Ndipo mmoja wa wale 12, aliyeitwa Yuda Iskariote, akaenda kwa wakuu wa makuhani na kuwauliza: “Mtanipa nini ili nimsaliti kwenu?” Wakakubaliana naye vipande 30 vya fedha.”

Mathayo 26:14, 15; 27:5
[Ukurasa wa 1601, 1604]

Biblia ilitabiri nini kuhusu nyakati zetu?

“Taifa litapigana na taifa na ufalme kupigana na ufalme . . . Mambo hayo yote ni mwanzo wa maumivu ya taabu.”

Mathayo 24:7, 8 [Ukurasa wa 1597]

“Manabii wengi wa uwongo watatokea na kuwapotosha wengi; na kwa sababu ya kuongezeka kwa uasi-sheria, upendo wa wengi utapoa.”

Mathayo 24:11, 12 [Ukurasa wa 1597]

“Mtakaposikia kuhusu vita na habari za vita, msiogope; lazima mambo hayo yatukie, lakini ule mwisho bado.”

Marko 13:7 [Ukurasa wa 1633]


“Kutakuwa na matetemeko makubwa ya ardhi, na magonjwa na upungufu wa chakula katika sehemu mbalimbali; pia kutakuwa na mambo yenye kuogopesha na ishara kubwa kutoka mbinguni.”

Luka 21:11 [Ukurasa wa 1688]

“Katika siku za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari zilizo ngumu ku-shughulika nazo. Kwa maana watu watakuwa wenye kujipenda wenye-we, wenye kupenda pesa, wenye kujidai, wenye majivuno, wakufuru, wasiotii wazazi, wasio na shukrani, wasio washikamanifu, wasio na upe-ndo wa asili, wasiotaka makubaliano yoyote, wachongezi, wasiojizua, wakali, wasiopenda wema, wasaliti, wenye vichwa vigumu, waliojaa kiburi, wanaopenda raha badala ya kumpenda Mungu, wakionekana kama watu wanaomwo-gopa Mungu lakini waki-zikana nguvu zake.”

2 Timotheo 3:1-5

[Ukurasa wa 1903]



Je, Mungu ndiye chanzo cha mateso yanayotupata?

“Mungu wa kweli hawezi kamwe kuwazia kutenda uovu, na Mweza-Yote hawezi kamwe kutenda kosa!”

Ayubu 34:10 [Ukurasa wa 876]

“Mtu akiwa chini ya jaribu, asiseme: ‘Mungu ananijaribu.’ Kwa maana Mungu hawezi kujaribiwa na mambo maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu yeyote.”

Yakobo 1:13 [Ukurasa wa 1928]

“[Tupeni] mahangaiko yenu yote juu yake, kwa sababu yeye anawajali ninyi.”

1 Petro 5:7 [Ukurasa wa 1939]

“Yehova hakawii kuhusiana na ahadi yake, kama watu fulani wanavyodhani, bali ni mwenye subira kwenu kwa sababu hataki yeyote aangamizwe bali hutaka wote wafikie toba.”

2 Petro 3:9 [Ukurasa wa 1944]

Kwa nini wanadamu huteseka?

“Sikuzote si wenye mbio wanaoshinda mbio, wala wenye nguvu hawashindi vita, wala wenye hekima hawapati chakula sikuzote, wala werevu hawawi na utajiri sikuzote, wala wenye ujuzi hawafanikiwi sikuzote, kwa sababu wakati na matukio yasiyotarajiwa huwapata wote.”

Mhubiri 9:11 [Ukurasa wa 1103]

“Kupitia mtu mmoja dhambi iliingia katika ulimwengu na kifo kupitia dhambi, basi kifo kikaenea kwa watu wote kwa sababu wote walikuwa wamefanya dhambi—.”

Waroma 5:12 [Ukurasa wa 1803]

“Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alifunuliwa, ili avunje kazi za Ibilisi.”

1 Yohana 3:8 [Ukurasa wa 1947]

“Ulimwengu mzima unakaa katika nguvu za yule mwovu.”

1 Yohana 5:19 [Ukurasa wa 1951]

Biblia inaahidi nini kuhusu wakati ujao?

“Waadilifu wataimiliki dunia, nao wataishi humo milele.”

Zaburi 37:29 [Ukurasa wa 930]

“Dunia inadumu milele.”

Mhubiri 1:4 [Ukurasa wa 1093]

“Atameza kifo milele, na Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atafuta kabisa machozi katika nyuso zote.”

Isaya 25:8 [Ukurasa wa 1156]

“Wakati huo macho ya vipofu yatafunguliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Wakati huo kilema ataruka kama paa, na ulimi wa bubu utapiga vigelegele vya shangwe. Kwa maana maji yatabubujika nyikani, na vijito katika jangwa tambarare.”

Isaya 35:5, 6 [Ukurasa wa 1173]

“Atafuta kila chozi kutoka katika macho yao, na kifo hakitakuwapo tena, wala maombolezo wala kilio wala maumivu hayatakuwapo tena. Mambo ya zamani yamepitilia mbali.”

Ufunuo 21:4 [Ukurasa wa 1981]

“Watajenga nyumba na kuishi ndani yake, nao watapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga na mtu mwingine akae ndani yake, wala hawatapanda na watu wengine wale. Kwa maana siku za watu wangu zitakuwa kama siku za mti, na watu wangu niliowachagua watafurahia kikamili kazi ya mikono yao.”

Isaya 65:21, 22 [Ukurasa wa 1225]



Ni nini hutokea mtu anapokufa?

“Roho yake hutoka, naye hurudi ardhini; siku hiyohiyo mawazo yake hupotea.”

Zaburi 146:4 [Ukurasa wa 1037]

“Walio hai wanajua kwamba watakufa, lakini waliokufa hawajui jambo lolote kamwe . . . Jambo lolote unalofanya kwa mkono wako, lifanye kwa nguvu zako zote, kwa sababu hakuna kazi wala mipango wala ujuzi wala hekima Kaburini, mahali unapokwenda.”

Mhubiri 9:5, 10 [Ukurasa wa 1102, 1103]

“[Yesu] akawaambia: ‘Rafiki yetu Lazaro amelala usingizi, lakini ninasafiri kwenda huko ili kumwamsha.’ Hata hivyo, Yesu alikuwa akizungumza kuhusu kifo cha Lazaro. Lakini walifikiri anasema kuhusu kupumzika katika usingizi. Ndipo Yesu akawaambia waziwazi: ‘Lazaro amekufa.’”

Yohana 11:11, 13, 14 [Ukurasa wa 1720]

Kuna tumaini gani kwa ajili ya wafu?

“Msishangazwe na jambo hili, kwa maana saa inakuja ambayo wote walio katika makaburi ya ukumbusho wataisikia sauti yake na kutoka.”

Yohana 5:28, 29 [Ukurasa wa 1708]

“Kutakuwa na ufufuo wa waadilifu na wasio waadilifu pia.”

Matendo 24:15 [Ukurasa wa 1787]

“Nami nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wakiwa wamesimama mbele ya kile kiti cha ufalme, na vitabu vya kukunjwa vikafunguliwa. Lakini kitabu kingine cha kukunjwa kikafunguliwa; hicho ni kitabu cha uzima. Wafu wakahukumiwa kutokana na yale mambo yaliyoandikwa katika vile vitabu kulingana na matendo yao. Na bahari ikawatoa wafu waliokuwa ndani yake, na kifo na Kaburi vikawatoa wafu waliokuwa ndani yake, nao wakahukumiwa kila mmoja kulingana na matendo yake.”

Ufunuo 20:12, 13 [Ukurasa wa 1980]

Biblia inasema nini kuhusu kufanya kazi?

“Je, umemwona mtu aliye stadi katika kazi yake? Atasimama mbele ya wafalme; hatasimama mbele ya watu wa kawaida.”

Methali 22:29 [Ukurasa wa 1076]


“Mwizi asiibe tena; badala yake afanye kazi kwa bidii, akifanya kazi njema kwa mikono yake, ili awe na kitu cha kumgawia mtu mwenye uhitaji.”

Waefeso 4:28 [Ukurasa wa 1871]

“Kila mtu anapaswa kula na kunywa na kufurahia kazi yake yote ngumu. Ni zawadi kutoka kwa Mungu.”

Mhubiri 3:13

[Ukurasa wa 1096]



Unawezaje kutumia vizuri pesa na mali zako?

“Anayependa raha atakuwa maskini; anayependa divai na mafuta hatakuwa tajiri.”

Methali 21:17 [Ukurasa wa 1074]

“Mkopaji ni mtumwa wa mkopeshaji.”

Methali 22:7 [Ukurasa wa 1075]

“Ni nani kati yenu anayetaka kujenga mnara ambaye haketi kwanza na kuhesabu gharama, ili aone kama ana kiasi cha kutosha kuukamilisha? La sivyo, ataweka msi-
ngi lakini ashindwe kumaliza, na wote wanaomtazama wataanza kumdhihaki, wakisema: ‘Mtu huyu alianza kujenga lakini akashindwa kumaliza.’”

Luka 14:28-30 [Ukurasa wa 1676]

“Waliposhiba akawaambia wanafunzi wake: ‘Kusanyeni vipande vilivyobaki, ili chochote kisipotee.’”

Yohana 6:12 [Ukurasa wa 1709]

Unawezaje kuwa na furaha?

“Ni afadhali kula mboga za majani mahali penye upendo kuliko kula ng’ombe dume aliyenoneshwa mahali penye chuki.”

Methali 15:17 [Ukurasa wa 1064]

“Mimi, Yehova, ni Mungu wako, ninayekufundisha ili ujifaidi mwenyewe, ninayekuongoza katika njia unayopaswa kutembea.”

Isaya 48:17 [Ukurasa wa 1198]

“Wenye furaha ni wale wanaotambua uhitaji wao wa kiroho, kwa kuwa Ufalme wa mbinguni ni wao.”

Mathayo 5:3 [Ukurasa wa 1563]

“Lazima umpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.”

Mathayo 22:39 [Ukurasa wa 1594]

“Kama vile mnavyotaka watu wawatendee ninyi, watendeeni vivyo hivyo.”

Luka 6:31 [Ukurasa wa 1656]

“Wenye furaha ni wale wanaolisikia neno la Mungu na kulishika!”


Luka 11:28 [Ukurasa wa 1669]

“Mtu anapokuwa na vitu vingi, uhai wake hautokani na vitu alivyo navyo.”

Luka 12:15 [Ukurasa wa 1671]

“Basi, tukiwa na chakula na mavazi, tutaridhika na vitu hivyo.”

1 Timotheo 6:8 [Ukurasa wa 1899]



“Kuna furaha zaidi katika kutoa kuliko ilivyo katika kupokea.”

Matendo 20:35
[Ukurasa wa 1780]

Unawezaje kukabiliana na mahangaiko?

“Mtupie Yehova mzigo wako, naye atakutegemeza. Hataruhusu kamwe mwadilifu aanguke.”

Zaburi 55:22 [Ukurasa wa 947]

“Mipango ya wenye bidii hakika huleta mafanikio, Lakini wote walio na haraka kwa hakika watakuwa maskini.”

Methali 21:5 [Ukurasa wa 1074]

“Usiogope, kwa maana mimi niko pamoja nawe. Usihangaike, kwa maana mimi ni Mungu wako. Nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, nitakushika kwelikweli kwa mkono wangu wa kuume wa uadilifu.”

Isaya 41:10 [Ukurasa wa 1183]

“Ni nani kati yenu ambaye kwa kuhangaika anaweza kurefusha uhai wake kwa mkono mmoja?”

Mathayo 6:27 [Ukurasa wa 1566]

“Basi, msihangaike kamwe kuhusu kesho, kwa maana kesho itakuwa na mahangaiko yake yenyewe. Kila siku ina matatizo yake ya kutosha.”

Mathayo 6:34 [Ukurasa wa 1567]

“Mhakikishe mambo muhimu zaidi.”

Wafilipi 1:10 [Ukurasa wa 1875]

“Msihangaikie kuhusiana na jambo lolote, bali katika kila jambo kwa sala na dua pamoja na kutoa shukrani, mjulisheni Mungu maombi yenu; na amani ya Mungu inayozi-di uelewaji wote itailinda mioyo yenu na nguvu zenu za akili kupitia Kristo Yesu.”

Wafilipi 4:6, 7 [Ukurasa wa 1879]



Biblia inawezaje kuisaidia familia yako?

WAUME/BABA

“Vivyo hivyo, waume wanapaswa kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Mwanamume anayempenda mke wake anajipenda mwenyewe, kwa maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake, bali huulisha na kuutunza . . . Kila mtu kati yenu anapaswa kumpenda mke wake kama anavyojipenda mwenyewe.”

Waefeso 5:28, 29, 33 [Ukurasa wa 1872]

“Nanyi akina baba, msiwe mkiwakasirisha watoto wenu, bali endeleeni kuwalea katika nidhamu na maagizo ya Yehova.”

Waefeso 6:4 [Ukurasa wa 1873]

WAKE

“Mke anapaswa kumheshimu sana mume wake.”

Waefeso 5:33 [Ukurasa wa 1872]

“Enyi wake, jitiisheni kwa waume zenu, kwa kuwa inafaa katika Bwana.”

Wakolosai 3:18 [Ukurasa wa 1884]

WATOTO

“Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika muungano na Bwana, kwa maana hilo ni jambo la uadilifu. ‘Mheshimu baba yako na mama yako,’ hiyo ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi: ‘Ili mambo yakuendee vema nawe ukae muda mrefu duniani.’”

Waefeso 6:1-3 [Ukurasa wa 1873]

“Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika kila jambo, kwa maana hilo humpendeza Bwana.”

Wakolosai 3:20 [Ukurasa wa 1884]

Unawezaje kumkaribia Mungu?

“Ee Msikiaji wa sala, watu wa kila aina watakuja.”

Zaburi 65:2 [Ukurasa wa 954]

“Mtumaini Yehova kwa moyo wako wote, wala usitegemee uelewaji wako mwenyewe. Katika njia zako zote mtambue yeye, naye atavinyoosha vijia vyako.”

Methali 3:5, 6 [Ukurasa wa 1045]

“Uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na yule uliyemtuma, Yesu Kristo.”

Yohana 17:3 [Ukurasa wa 1730]

“Kwa hakika, [Mungu] hayuko mbali na kila mmoja wetu.”

Matendo 17:27 [Ukurasa wa 1774]

“Hili ndilo ninaloendelea kusali, kwamba upendo wenu uwe mwingi zaidi na zaidi pamoja na ujuzi sahihi na utambuzi kamili.”

Wafilipi 1:9 [Ukurasa wa 1875]

“Ikiwa yeyote kati yenu anakosa hekima, na aendeleo kumwomba Mungu, kwa maana yeye huwapa wote kwa ukarimu na bila kushutumu, naye atapewa.”

Yakobo 1:5 [Ukurasa wa 1928]

“Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Safisheni mikono yenu, ninyi watenda dhambi, na takaseni mioyo yenu, ninyi mnaositasita.”

Yakobo 4:8 [Ukurasa wa 1932]

“Kwa maana kumpenda Mungu humaanisha hivi, kwa-mba tushike amri zake; na bado amri zake si mzigo mzito.”

1 Yohana 5:3 [Ukurasa wa 1950]

Vitabu vya Biblia vina ujumbe gani?

MAANDIKO YA KIEBRANIA (“AGANO LA KALE”)

PENTATEUKI (VITABU 5):

Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu,
Kumbukumbu la Torati

Kuanzia uumbaji mpaka kuanzishwa kwa taifa la kale la Israeli

VITABU VYA KIHISTORIA (VITABU 12):

Yoshua, Waamuzi, Ruthu

Kuanzia wakati Waisraeli walipoingia katika Nchi ya Ahadi na matukio yaliyofuata

1 na 2 Samweli, 1 na 2 Wafalme, 1 na 2 Mambo ya Nyakati

Historia ya taifa la Israeli kufikia kuharibiwa kwa Yerusalemu

Ezra, Nehemia, Esta

Historia ya Wayahudi baada ya kurudi kutoka utekwani Babiloni

VITABU VYA MASHAIRI (VITABU 5):

Ayubu, Zaburi, Methali, Mhubiri, Wimbo wa Sulemani
Mkusanyo wa maneno ya hekima na nyimbo

VITABU VYA UNABII (VITABU 17):

Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli, Danieli, Hosea,
Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki,
Sefania, Hagai, Zekaria, Malaki

Unabii, au utabiri unaohusu watu wa Mungu

MAANDIKO YA KIGIRIKI YA KIKRISTO (“AGANO JIPYA”)

VITABU VINNE VYA INJILI (VITABU 4):

Mathayo, Marko, Luka, Yohana

Historia ya maisha na huduma ya Yesu

MATENDO YA MITUME (KITABU 1):

Historia ya mwanzo wa kutaniko la Kikristo na kazi ya kuhubiri

BARUA (VITABU 21):

Waroma, 1 na 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso,

Wafilipi, Wakolosai, 1 na 2 Wathesalonike

Barua zilizotumwa kwa makutaniko

mbalimbali ya Kikristo

1 na 2 Timotheo, Tito, Filemoni

Barua zilizotumwa kwa Mkristo

mmoja-mmoja

Waebrania, Yakobo, 1 na 2 Petro,

1, 2, na 3 Yohana, Yuda

Barua zilizotumwa kwa

Wakristo kwa ujumla

UFUNUO (KITABU 1):

Mfuatano wa maono ya unabii aliyopewa mtume Yohana

Unawezaje kunufaika zaidi unaposoma Biblia?

UNAPOSOMA BIBLIA YAKO JIULIZE MASWALI YAFUATAYO:

Jambo hili linanifundisha nini kumhusu Yehova Mungu?

Sehemu hii ya Maandiko inahusianaje na ujumbe wa Biblia?

Ninawezaje kutumia habari hii maishani mwangu?

Ninawezaje kutumia maandiko haya kuwasaidia wengine?

“Neno lako ni taa ya mguu wangu, na nuru ya njia yangu.”

Zaburi 119:105

[Ukurasa wa 1018]



UTANGULIZI

Biblia Takatifu ni ujumbe wa Mungu ulioandikwa kwa ajili yetu sote. Ni lazima tuji-funze Biblia ili tumjue Mtungaji wake. (Yohana 17:3; 2 Timotheo 3:16) Katika Biblia, Yehova Mungu hufunua kusudi lake kwa ajili ya wanadamu na kwa ajili ya dunia, makao ya wanadamu.—Mwanzo 3:15; Ufunuo 21:3, 4.

Hakuna kitabu kingine chochote kilicho na nguvu za kubadili maisha ya watu kama Biblia. Biblia hutuchochea kutafakari kuhusu sifa za Yehova kama vile upendo, re-hema, na huruma. Huwapa watu tumaini na kuwasaidia kuvumilia hata mateso ma-kali sana. Nayo inaendelea kufunua mambo ya ulimwengu huu yasiyopatana na mapenzi makamilifu ya Mungu.—Zaburi 119:105; Waebrania 4:12; 1 Yohana 2:15-17.

Mwanzoni Biblia iliandikwa katika lugha ya Kiebrania, Kiaramu, na Kigiriki, lakini sasa imetafsiriwa, ikiwa nzima au kwa sehemu, katika lugha zaidi ya 3,000 hivi. Ndicho kitabu kilichotafsiriwa katika lugha nyingi zaidi na kusambazwa kwa wingi sana katika historia. Na jambo hilo halitushangazi. Unabii wa Biblia unasema hivi: “Hii habari njema ya Ufalme [ambao ndio ujumbe wa msingi wa Biblia] itahubiriwa katika dunia yote inayokaliwa ili kuwa ushahidi kwa mataifa yote, na ndipo ule mwi-sho utakapokuja.”—Mathayo 24:14.

Kwa kuwa tunatambua umuhimu wa ujumbe wa Biblia, tumeboresha tafsiri hii tuki-wa na heshima kubwa sana kuelekea ujumbe wa Biblia. Tunatambua kwamba tuna wajibu mzito sana wa kuwasilisha ujumbe wake kwa usahihi. Toleo hili lililoreke-bishwa linategemea msingi mzuri uliowekwa na matoleo ya awali ya *New World Translation of the Holy Scriptures*, Biblia iliyotolewa kwa mara ya kwanza zaidi ya miaka 60 iliyopita. Hata hivyo, lugha ya Kiingereza imebadilika katika muda wa miaka 50 iliyopita. Mabadiliko hayo ndiyo yaliyofanya washiriki wa sasa wa Hal-mashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya waanze kazi kubwa ya kuibore-sha. Lengo letu lilikuwa kutayarisha tafsiri inayowasilisha kwa uaminifu mawazo ya maandishi ya awali na ambayo inaeleweka na kusomeka kwa urahisi. Makala za Nyongeza zenye kichwa “Kanuni za Kutafsiri Biblia,” “Sehemu za Toleo Hili,” na “Ji-nsi Biblia Ilivyotufikia” zinazungumzia baadhi ya mambo yaliyoiboreshwa katika to-leo hili kuhusiana na lugha.

Wale wanaompenda Yehova Mungu na kumwabudu wanatamani kuwa na tafsiri sa-hihi na inayoeleweka ya Neno la Mungu. (1 Timotheo 2:4) Kwa hiyo, tumetoa to-leo hili lililorekebisha katika Kiingereza tukikusudia litafsiriwe katika lugha nyingi iwezekanavyo. Tunatumaini na kusali kwamba, wewe msomaji mpendwa, utanufai-ka na toleo hili la Maandiko Matakatifu unapojitahidi ‘kumtafuta Mungu na kwa kweli umpate.’—Matendo 17:27.

Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya
Agosti 2013

Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya katika Kiswahili ilitolewa mwaka wa 2003. Toleo hili la Kiswahili la mwaka wa 2017 ambalo ndilo la karibuni zaidi lime-rekebisha kwa kutegemea Biblia ya Kiingereza ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* iliyo-rekebisha mwaka wa 2013, na lina sehemu zote zilizo katika tafsiri ya Kiingereza.

MAJINA NA MPANGILIO WA VITABU

VYA MAANDIKO YA KIEBRANIA NA KIARAMU

KITABU	UFUPISHO	UKU.	KITABU	UFUPISHO	UKU.
Mwanzo	Mwa	41	Mhubiri	Mhu	1092
Kutoka	Kut	126	Wimbo wa Sulemani	Wim	1106
Mambo ya Walawi	Law	197	Isaya	Isa	1116
Hesabu	Hes	249	Yeremia	Yer	1228
Kumbukumbu la Torati	Kum	320	Maombolezo	Omb	1336
Joshua	Yos	380	Ezekieli	Eze	1348
Waamuzi	Amu	418	Danieli	Da	1437
Ruthu	Ru	457	Hosea	Ho	1465
1 Samweli	1Sa	463	Yoeli	Yoe	1481
2 Samweli	2Sa	517	Amosi	Amo	1488
1 Wafalme	1Fa	564	Obadia	Oba	1501
2 Wafalme	2Fa	618	Yona	Yon	1503
1 Mambo ya Nyakati	1Nya	670	Mika	Mik	1506
2 Mambo ya Nyakati	2Nya	717	Nahumu	Nah	1517
Ezra	Ezr	776	Habakuki	Hab	1521
Nehemia	Ne	793	Sefania	Sef	1526
Esta	Est	817	Hagai	Hag	1532
Ayubu	Ayu	830	Zekaria	Zek	1534
Zaburi	Zb	889	Malaki	Mal	1550
Methali	Met	1040			

VYA MAANDIKO YA KIGIRIKI YA KIKRISTO

KITABU	UFUPISHO	UKU.	KITABU	UFUPISHO	UKU.
Mathayo	Mt	1556	1 Timotheo	1Ti	1893
Marko	Mk	1608	2 Timotheo	2Ti	1900
Luka	Lu	1641	Tito	Tit	1905
Yohana	Yoh	1697	Filemoni	Flm	1908
Matendo	Mdo	1739	Waebrania	Ebr	1910
Waroma	Ro	1795	Yakobo	Yak	1927
1 Wakorintho	1Ko	1819	1 Petro	1Pe	1933
2 Wakorintho	2Ko	1842	2 Petro	2Pe	1940
Wagalatia	Gal	1858	1 Yohana	1Yo	1945
Waefeso	Efe	1866	2 Yohana	2Yo	1951
Wafilipi	Flp	1874	3 Yohana	3Yo	1952
Wakolosai	Kol	1880	Yuda	Yud	1953
1 Wathesalonike	1Th	1886	Ufunuo	Ufu	1955
2 Wathesalonike	2Th	1891			

Orodha ya Vitabu vya Biblia	1984	Nyongeza A	2037
Fahirisi ya Maneno ya Biblia	1986	Nyongeza B	2085
Kamusi ya Maneno ya Biblia	2012		

MWANZO

YALIYOMO

- 1 Uumbaji wa mbingu na dunia (1, 2)
Siku sita za kuitayarisha dunia (3-31)
Siku ya 1: nuru; mchana na usiku (3-5)
Siku ya 2: anga (6-8)
Siku ya 3: nchi kavu na mimea (9-13)
Siku ya 4: mianga ya mbinguni (14-19)
Siku ya 5: samaki na ndege (20-23)
Siku ya 6: wanyama wa nchi kavu na wanadamu (24-31)
- 2 Mungu apumzika siku ya saba (1-3)
Yehova Mungu, Muumbaji wa mbingu na dunia (4)
Mwanamume na mwanamke katika bustani ya Edeni (5-25)
Mtu aumbwa kutokana na mavumbi (7)
Mti uliokatazwa wa ujuzi (15-17)
Kuumbwa kwa mwanamke (18-25)
- 3 Mwanzo wa dhambi ya wanadamu (1-13)
Uwongo wa kwanza (4, 5)
Yehova awahukumu waasi (14-24)
Uzao wa mwanamke watabiriwa (15)
Kufukuzwa Edeni (23, 24)
- 4 Kaini na Abeli (1-16)
Wazao wa Kaini (17-24)
Sethi na Enoshi mwanawe (25, 26)
- 5 Kuanzia Adamu mpaka Noa (1-32)
Adamu azaa wana na mabinti (4)
Enoko alitembea na Mungu (21-24)
- 6 Wana wa Mungu wajichukulia wake duniani (1-3)
Wanefili wazaliwa (4)
Uovu wa wanadamu wamhuzunisha Yehova (5-8)
Noa aagizwa ajenge safina (9-16)
Mungu atangaza kuja kwa Gharika (17-22)
- 7 Kuingia ndani ya safina (1-10)
Gharika duniani kote (11-24)
- 8 Maji ya Gharika yapungua (1-14)
Njiwa atumwa (8-12)
Kutoka ndani ya safina (15-19)
Ahadi ya Mungu kuhusu dunia (20-22)
- 9 Maagizo kwa wanadamu wote (1-7)
Sheria kuhusu damu (4-6)
- Agano la upinde (8-17)
Unabii mbalimbali kuhusu wazao wa Noa (18-29)
- 10 Orodha ya mataifa (1-32)
Wazao wa Yafethi (2-5)
Wazao wa Hamu (6-20)
Nimrodi ampinga Yehova (8-12)
Wazao wa Shemu (21-31)
- 11 Mnara wa Babeli (1-4)
Yehova avuruga lugha (5-9)
Kuanzia Shemu hadi Abramu (10-32)
Familia ya Tera (27)
Abramu ahama Uru (31)
- 12 Abramu ahama Harani na kwenda Kanaani (1-9)
Ahadi ya Mungu kwa Abramu (7)
Abramu na Sarai katika nchi ya Misri (10-20)
- 13 Abramu arudi Kanaani (1-4)
Abramu na Loti watengana (5-13)
Mungu arudia ahadi aliyompa Abramu (14-18)
- 14 Abramu amwokoia Loti (1-16)
Melkizedeki ambariki Abramu (17-24)
- 15 Agano kati ya Mungu na Abramu (1-21)
Miaka 400 ya mateso yatabiriwa (13)
Mungu arudia ahadi aliyompa Abramu (18-21)
- 16 Hagari na Ishmaeli (1-16)
- 17 Abrahamu atakuwa baba wa mataifa mengi (1-8)
Abramu apewa jina jipya, Abrahamu (5)
Agano la kutahiri (9-14)
Sarai apewa jina jipya, Sara (15-17)
Aahidiwa kumzaa mwana aitwaye Isaka (18-27)
- 18 Malaika watatu wamtembelea Abrahamu (1-8)
Sara aahidiwa kuzaa mwana; Sara acheka (9-15)
Abrahamu amsihi Mungu asiangamize Sodoma (16-33)
- 19 Loti atembelea na malaika (1-11)
Loti na familia yake waagizwa waondoke (12-22)

- Majiji ya Sodom na Gomora yaharihiwa (23-29)
 Mke wa Loti awa nguzo ya chumvi (26)
 Loti na mabinti wake (30-38)
 Mwanzo wa Wamoabu na Waamoni (37, 38)
- 20 Sara aokolewa kutoka mikononi mwa Abimeleki (1-18)
- 21 Isaka azaliwa (1-7)
 Ishmaeli amdhihaki Isaka (8, 9)
 Hagari na Ishmaeli wafukuzwa (10-21)
 Agano kati ya Abrahamu na Abimeleki (22-34)
- 22 Abrahamu aambiwa amtoe Isaka (1-19)
 Uzao wa Abrahamu utaleta baraka (15-18)
 Familia ya Rebeka (20-24)
- 23 Kifo cha Sara na mahali alipozikwa (1-20)
- 24 Isaka atafutiwa mke (1-58)
 Rebeka aenda kukutana na Isaka (59-67)
- 25 Abrahamu aoa tena (1-6)
 Kifo cha Abrahamu (7-11)
 Wana wa Ishmaeli (12-18)
 Yakobo na Esau wazaliwa (19-26)
 Esau auza haki yake ya mzaliwa wa kwanza (27-34)
- 26 Isaka na Rebeka wakiwa Gerari (1-11)
 Mungu amhakikishia Isaka kwamba atatimiza ahadi yake (3-5)
 Wagombania visima (12-25)
 Agano kati ya Isaka na Abimeleki (26-33)
 Wake wawili Wahiti wa Esau (34, 35)
- 27 Yakobo abarikiwa na Isaka (1-29)
 Esau atafuta baraka lakini akosa kutubu (30-40)
 Esau amchukia sana Yakobo (41-46)
- 28 Isaka amtuma Yakobo
 Padan-aramu (1-9)
 Ndoto ya Yakobo akiwa Betheli (10-22)
 Mungu amhakikishia Yakobo kwamba atatimiza ahadi yake (13-15)
- 29 Yakobo akutana na Raheli (1-14)
 Yakobo ampenda Raheli (15-20)
 Yakobo amwoa Lea na pia Raheli (21-29)
 Wana wanne wa Yakobo waliozaliwa na Lea: Rubeni, Simeoni, Lawi, na Yuda (30-35)
- 30 Bilha amzaa Dani na Naftali (1-8)
 Zilpa amzaa Gadi na Asheri (9-13)
 Lea amzaa Isakari na Zabuloni (14-21)
 Raheli amzaa Yosefu (22-24)
 Mifugo ya Yakobo yaongezeka (25-43)
- 31 Yakobo aenda kwa sira Kanaani (1-18)
 Labani amfikia Yakobo (19-35)
 Agano kati ya Yakobo na Labani (36-55)
- 32 Malaika wakutana na Yakobo (1, 2)
 Yakobo ajitayarisha kukutana na Esau (3-23)
 Yakobo apigana mweleka na malaika (24-32)
 Yakobo apewa jina jipya, Israeli (28)
- 33 Yakobo akutana na Esau (1-16)
 Yakobo asafiri kwenda Shekemu (17-20)
- 34 Dina abakwa (1-12)
 Wana wa Yakobo watenda kwa udanganyifu (13-31)
- 35 Yakobo aondoa miungu ya kigeni (1-4)
 Yakobo arudi Betheli (5-15)
 Benjamini azaliwa; Raheli afa (16-20)
 Wana 12 wa Israeli (21-26)
 Kifo cha Isaka (27-29)
- 36 Wazao wa Esau (1-30)
 Wafalme na mashehe wa Edomu (31-43)
- 37 Ndoto za Yosefu (1-11)
 Yosefu na ndugu zake wenye wivu (12-24)
 Yosefu auzwa utumwani (25-36)
- 38 Yuda na Tamari (1-30)
- 39 Yosefu katika nyumba ya Potifa (1-6)
 Yosefu ampinga mke wa Potifa aliyekuwa akimshawishi (7-20)
 Yosefu akiwa gerezani (21-23)
- 40 Yosefu aeleza maana ya ndoto za wafungwa wenzake (1-19)
 'Ni kazi ya Mungu kueleza maana ya ndoto' (8)
 Karamu ya siku ya kuzaliwa kwa Farao (20-23)
- 41 Yosefu aeleza maana ya ndoto za Farao (1-36)
 Yosefu akwezwa na Farao (37-46a)
 Yosefu awekwa kuwa msimamizi wa chakula (46b-57)
- 42 Ndugu za Yosefu waenda Misri (1-4)
 Yosefu akutana na ndugu zake na kuwajaribu (5-25)

- Ndugu zake warudi nyumbani kwa Yakobo (26-38)
- 43 Ndugu za Yosefu warudi Misri mara ya pili wakiwa na Benjamini (1-14)
Yosefu akutana tena na ndugu zake (15-23)
Yosefu ala na kunywa na ndugu zake (24-34)
- 44 Kikombe cha fedha cha Yosefu chapatikana katika mfuko wa Benjamini (1-17)
Yuda asihi Benjamini aachiliwe (18-34)
- 45 Yosefu ajitambulisha (1-15)
Ndugu za Yosefu warudi kumchukua Yakobo (16-28)
- 46 Yakobo na familia yake wahamia Misri (1-7)
Majina ya waliohamia Misri (8-27)
Yosefu na Yakobo wakutana Gosheni (28-34)
- 47 Yakobo akutana na Farao (1-12)
Usimamizi wenye hekima wa Yosefu (13-26)
Israeli aishi Gosheni (27-31)
- 48 Yakobo awabariki wana wawili wa Yosefu (1-12)
Efraimu apata baraka kubwa zaidi (13-22)
- 49 Unabii wa Yakobo alipokuwa akifa (1-28)
Shilo atatoka Yuda (10)
Maagizo ya kumzika Yakobo (29-32)
Kifo cha Yakobo (33)
- 50 Yosefu amzika Yakobo Kanaani (1-14)
Yosefu awahakikishia ndugu zake kwamba amewasamehe (15-21)
Siku za mwisho za Yosefu na kifo chake (22-26)
Amri ya Yosefu kuhusu mifupa yake (25)

1 Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na dunia.^a

2 Sasa dunia haikuwa na umbo nayo ilikuwa tupu,* na giza lilikuwa juu ya kilindi cha maji,^{#b} na nguvu ya utendaji ya Mungu^{Δc} ilikuwa ikienda huku na huku juu ya maji.^d

3 Na Mungu akasema: "Kuwe na nuru." Basi kukawa na nuru.^e **4** Baada ya hayo, Mungu akaona kwamba nuru ilikuwa nzuri, na Mungu akaanza kuitenganisha nuru na giza. **5** Mungu akaiita nuru Mchana, lakini giza akaliita Usiku.^f Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya kwanza.

6 Kisha Mungu akasema: "Na kuwe na anga^g katikati ya maji, na anga liyatenganishe maji na maji."^h **7** Ndipo Mu-

1:2 * Au "ukiwa." # Au "maji yenye nguvu." Δ Au "roho ya Mungu."

SURA YA 1

a Zb 102:25
Isa 42:5
Isa 45:18
Ro 1:20
Ebr 1:10
Ufu 4:11
Ufu 10:6

b Met 8:27, 28

c Zb 33:6
Isa 40:26

d Zb 104:5, 6

e Isa 45:7
2Ko 4:6

f Mwa 8:22

g Mwa 1:20

h 2Pe 3:5

Safu ya 2

a Mwa 7:11
Met 8:27, 28

b Ayu 38:8, 11
Zb 104:6-9
Zb 136:6

c Zb 95:5

d Met 8:29

e Kum 32:4

f Zb 104:14

ngu akatengeneza anga na kuyatenganisha maji yaliyo chini ya anga na maji yaliyo juu ya anga.^a Na ikawa hivyo. **8** Mungu akaiita anga Mbingu. Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya pili.

9 Kisha Mungu akasema: "Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, na nchi kavu itokee."^b Na ikawa hivyo. **10** Mungu akaiita nchi kavu Dunia,^c lakini mkusanyiko wa maji, akauita Bahari.^d Na Mungu akaona kuwa ni vyema.^e **11** Kisha Mungu akasema: "Dunia na ichipushe majani, mimea inayozaa mbegu na miti ya matunda inayozaa matunda kulingana na aina zake, miti inayozaa matunda yenye mbe-gu duniani." Na ikawa hivyo. **12** Dunia ikaanza kuchipusha majani, mimea inayozaa mbe-gu^f na miti inayozaa matunda

yenye mbegu, kulingana na aina zake. Kisha Mungu akao-na kuwa ni vyema. **13** Ika-wa jioni, ikawa asubuhi, siku ya tatu.

14 Kisha Mungu akasema: “Na kuwe na mianga*^a kati-ka anga la mbingu ili itenganishe mchana na usiku,^b nayo itakuwa ishara ya kuonyesha majira na siku na mia-ka.^c **15** Itakuwa mianga kati-ka anga la mbingu ili kuangazia dunia.” Na ikawa hivyo. **16** Ndipo Mungu akatengeneza mianga miwili mikubwa, mwanga mkubwa zaidi wa kutawala mchana^d na mwanga mdogo wa kutawala usiku, na pia nyota.^e **17** Basi Mungu akaiweka katika anga la mbingu ili iangazie dunia **18** na kutawala wakati wa mchana na wakati wa usiku na kute-nganisha nuru na giza.^f Mungu akaona kuwa ni vyema. **19** Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya nne.

20 Kisha Mungu akasema: “Maji na yajae viumbe walio* hai, na viumbe wanaoruka waruke juu ya dunia katika anga la mbingu.”^g **21** Mungu akaumba viumbe waku-bwa* wa baharini na viumbe wote walio hai waendao na waliojaa majini kulingana na aina zao na kila kiumbe mwe-nye mabawa anayeruka, ku-lingana na aina yake. Mungu akaona kuwa ni vyema. **22** Basi Mungu akawabariki akisema: “Zaeni, muwe wengi na kujaza maji ya bahari,^h na viumbe wanaoruka wawe wen-gi duniani.” **23** Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya tano.

1:14 *Au “taa.” 1:20 *Au “nafsi zilizo.”
#Au “angani.” 1:21 *Au “wanyama wa-kubwa sana.”

SURA YA 1

a Kum 4:19

b Zb 104:19

c Mwa 8:22

d Zb 136:7,8

e Zb 8:3
Yer 31:35

f Zb 74:16

g Mwa 2:19

h Ne 9:6
Zb 104:25

Safu ya 2

a Mwa 2:19

b Met 8:30
Yoh 1:3
Kol 1:16

c 1Ko 11:7

d Mwa 5:1
Yak 3:9

e Mwa 9:2

f Zb 139:14
Mt 19:4
Mk 10:6
1Ko 11:7,9

g Mwa 9:1

h Mwa 2:15

i Zb 8:4,6

j Mwa 9:3
Zb 104:14
Mdo 14:17

24 Kisha Mungu akasema: “Dunia na itokeze viumbe walio* hai kulingana na aina zao, wanyama wa kufugwa na wanyama wanaotambaa[#] na wanyama wa mwituni kulingana na aina zao.”^a Na ikawa hivyo. **25** Kisha Mungu akau-amba wanyama wa mwituni kulingana na aina zao na wanyama wa kufugwa kulingana na aina zao na wanyama wote wanaotambaa kulingana na aina zao. Mungu akaona kuwa ni vyema.

26 Kisha Mungu akasema: “Na tufanye^b mtu kwa mfa-no^c wetu, kulingana na sura^d yetu, nao watawale samaki wa baharini na viumbe wanaoruka angani na wanyama wa ku-fugwa na dunia yote na kila mnyama anayetambaa du-niani.”^e **27** Basi Mungu aka-muumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mu-ngu alimuumba; mwanamume na mwanamke aliwau-mba.^f **28** Zaidi ya hilo, Mungu akawabariki, na Mungu akawaambia: “Zaeni, muwe wengi, muijaze dunia^g na kui-tiisha,^h na mtawaleⁱ samaki wa baharini na viumbe wanaoruka angani na kila kiumbe ali-ye hai anayetembea duniani.”

29 Kisha Mungu akasema: “Tazama nimewapa kila mmea duniani pote unaozaa mbegu na kila mti unaozaa matunda yenye mbegu. Itakuwa chaku-la chenu.^j **30** Na kila mnyama wa mwituni na kila kiumbe anayeruka angani na kila

1:24 *Au “nafsi.” #Au “wanyama wae-ndao,” inaonekana wanatia ndani wa-nyama wanaotambaa na jamii nyingine za wanyama zilizo tofauti na jamii nyi-nginezo.

kiumbe mwenye uhai* anayetembea duniani, nimempa mi-mea yote ya kijani iwe chaku-la^a chake.” Ikawa hivyo.

31 Baada ya hayo Mungu akaona kila kitu alichoumba, na tazama! kilikuwa chema sana.^b Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya sita.

2 Basi mbingu na dunia na kila kitu kilichomo vika-kamilika.*^c **2** Na kufikia siku ya saba, Mungu alikuwa amemaliza kazi aliyokuwa akifanya, naye akaanza kupumzika siku ya saba kutoka katika kazi yake yote aliyokuwa amefanya.^d **3** Na Mungu akaibariki siku ya saba na kuitanga-za kuwa takatifu, kwa kuwa katika siku hiyo Mungu amekuwa akipumzika kutokana na kazi yake yote ya kuumba, vyote alivyokusudia kuumba.

4 Hii ndiyo historia ya mbingu na dunia wakati zilipoumbwa, siku ambayo Yehova* Mungu aliumba dunia na mbingu.^e

5 Dunia bado haikuwa na kichaka chochote na hakuna mmea wowote uliokuwa umeanza kuchipuka, kwa sababu Yehova Mungu hakuwa amefanya mvua inyeshe duniani na hapakuwa na mtu wa kuilima ardhi. **6** Lakini ukungu ulikuwa ukipanda kutoka duniani, nao uliinyesha ardhi yote.

7 Kisha Yehova Mungu akamuumba mtu kutokana na mavumbi^f ya ardhi na kupuliza katika mianzi ya pua yake pu-

1:30 *Au “ambaye ni nafsi hai.” 2:1 *Tnn., “na jeshi lake lote likakamilika.” 2:4 *Hili ndilo andiko la kwanza kutaja jina la pekee la Mungu, יהוה (YHWH). Angalia Nyongeza A4.

SURA YA 1

a Zb 147:9
Mt 6:26

b Kum 32:4
Zb 104:24
1Ti 4:4

SURA YA 2

c Ne 9:6
Zb 146:6

d Kut 31:17
Ebr 4:4

e Isa 45:18

f Mwa 3:19
Zb 103:14
Mhu 3:20

Safu ya 2

a Mwa 7:22
Isa 42:5
Mdo 17:25

b 1Ko 15:45, 47

c Mwa 2:15
Mwa 3:23

d Mwa 1:26

e Mwa 3:22, 24
Ufu 2:7

f Mwa 2:17

g Da 10:4

h Mwa 10:8, 11

i Mwa 15:18
Kum 11:24

j Mwa 1:28
Mwa 2:8
Zb 115:16

k Mwa 2:8, 9
Mwa 3:2

l Mwa 3:19
Zb 146:4
Mhu 9:5, 10
Eze 18:4
Ro 5:12
1Ko 15:22

mzi ya uhai,^a na mtu huyo akawa mtu aliye hai.*^b **8** Zaidi ya hilo, Yehova Mungu akapanda bustani kule Edeni,^c kuelekea mashariki; na humo akamweka huyo mtu aliye-muumba.^d **9** Kwa hiyo Yehova Mungu akachipusha ardhi ni kila mti wenye kupendeza macho na unaofaa kwa chakula na pia mti wa uzima^e katikati ya bustani na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.^f

10 Sasa kulikuwa na mto uliotiririka kutoka Edeni ili kuinyesha bustani, na kutoka huko uligawanyika na kuwa mito minne.* **11** Jina la mto wa kwanza ni Pishoni; ndio unaozunguka nchi yote ya Havila, ambako kuna dhahabu. **12** Dhahabu ya nchi hiyo ni nzuri. Pia kuna uto-mvu wa mbedola na madini ya shohamu. **13** Jina la mto wa pili ni Gihoni; ndio unaozunguka nchi yote ya Kushi. **14** Jina la mto wa tatu ni Hidekali;*^g ndio unaoelekea upande wa mashariki wa Ashuru.^h Na mto wa nne ni Efrati.ⁱ

15 Yehova Mungu akamchukua huyo mtu na kumweka katika bustani ya Edeni ili ailime na kuitunza.^j

16 Pia, Yehova Mungu akampa huyo mtu amri hii: “Unaweza kula matunda ya kila mti katika bustani mpaka ushibe.^k **17** Lakini kuhusu mti wa ujuzi wa mema na mabaya, usile matunda yake, kwa maa-na siku utakapokula matunda yake hakika utakufa.”^l

2:7 *Au “nafsi hai.” Kiebrania, *ne'phesh*, ambalo kihalisi linamaanisha “kiumbe anayepumua.” Angalia Kamusi, uke. 2012. **2:10** *Tnn., “na kuwa vi-chwa vinne.” **2:14** *Au “Tigri.”

18 Kisha Yehova Mungu akasema: “Si vema mwanamume huyu aendelee kuwa peke yake. Nitamuambia msaidizi, awe kikamilisho chake.”^a

19 Sasa Yehova Mungu aliumba kutoka mavumbini kila mnyama wa mwituni na kila kiumbe anayeruka angani, naye akaanza kuwaleta kwa mtu huyo ili aamue jina atakalompaa kila kiumbe; na jina lolote ambalo mtu huyo alimpa kila kiumbe aliyehai, likawa jina lake.^b

20 Basi mtu huyo akawapa majina wanyama wote wa kufugwa na viumbe wote wanaoruka angani na kila mnyama wa mwituni, lakini mwanamume huyo hakuwa na msaidizi ambaye angekuwa kikamilisho chake. **21** Kwa hiyo Yehova Mungu akamletea mwanamume huyo usingizi mzito, na alipokuwa akilala, akachukua ubavu wake mmoja na kufunika nyama mahali hapo. **22** Na Yehova Mungu akaufanya ubavu aliochukua kutoka kwa mwanamume uwe mwanamke, naye akamletea kwa mwanamume huyo.^c

23 Ndipo mwanamume huyo akasema:

“Hatimaye huyu ni mfupa wa mifupa yangu
Na nyama ya nyama yangu.
Huyu ataitwa Mwanamke,
Kwa sababu alitolewa^d katika mwanamume.”

24 Ndiyo sababu mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye atashikamana* na mke wake, nao watakuwa mwili mmoja.^e

25 Na wote wawili wakaendelea kuwa uchi,^f huyo mwana-

SURA YA 2

a 1Ko 11:8,9
1Ti 2:13

b Mwa 1:26

c Mk 10:9
1Ti 2:13

d 1Ko 11:8

e Mal 2:16
Mt 19:5
Mk 10:7,8
Ro 7:2
1Ko 6:16
Efe 5:31
Ebr 13:4

f Mwa 3:7

Safu ya 2

SURA YA 3

a 2Ko 11:3
Ufu 12:9
Ufu 20:2

b Mwa 2:17

c Mwa 2:16

d Mwa 2:8,9

e Yoh 8:44
1Yo 3:8

f Mwa 3:22

g 2Ko 11:3
1Ti 2:14
Yak 1:14,15

h Ro 5:12

i Mwa 3:21

mume na mke wake; lakini hawakuona aibu.

3 Basi nyoka^a alikuwa mwenye kujihadhari* kuliko wanyama wote wa mwituni walioumbwa na Yehova Mungu. Kwa hiyo, akamuuliza mwanamke: “Je, ni kweli kwamba Mungu alisema msile matunda ya kila mti wa bustani?”^b

2 Mwanamke akamjibu nyoka: “Tunaweza kula matunda ya miti ya bustani.^c **3** Lakini Mungu amesema hivi kuhusu matunda ya mti ulio katikati ya bustani:^d ‘Msiyale, wala msiyaguse; la si vyo mtakufa.’” **4** Ndipo nyoka akamwambia mwanamke: “Hakika hamtakufa.^e **5** Kwa maana Mungu anajua kwamba siku ileile mtakapokula matunda ya mti huo, macho yenu yatafunguliwa nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.”^f

6 Kwa hiyo, mwanamke akaona kwamba mti huo ulifaa kwa chakula na kwamba ulikuwa kitu kinachotamaniwa kwa macho, naam, mti huo ulipendeza macho. Basi akaanza kuchuma matunda ya mti huo na kula.^g Baadaye, akampa pia mume wake baadhi ya matunda hayo alipokuwa pamoja naye, naye akaanza kula.^h **7** Ndipo macho yao wote wawili yakafunguliwa, nao wakatambua kwamba walikuwa uchi. Kwa hiyo wakayafunga pamoja majani ya mtini na kujitengeneza mavazi ya kujifunika kiunoni.ⁱ

8 Baadaye wakasikia sauti ya Yehova Mungu alipokuwa akitembea katika busta-

2:24 *Au “ataendelea kuwa.”

3:1 *Au “mjanja; mwenye hila.”

ni wakati ambapo kuna upepo mtulivu, na mwanamume huyo na mke wake wakajificha katikati ya miti ya bustani kutoka mbele za uso wa Yehova Mungu. **9** Na Yehova Mungu akamwita huyo mwanamume tena na tena na kumuuliza: “Uko wapi?” **10** Mwishowe akajibu: “Niliisikia sauti yako katika bustani, lakini niliogopa kwa sababu nilikuwa uchi, basi nikajificha.” **11** Ndipo Mungu akamuuliza: “Ni nani aliyekwambia uko uchi?”^a Je, umekula matunda ya mti niliokuamuru usile?”^b **12** Mwanamume huyo akasema: “Mwanamke uliyenipa nikae naye, alinipa tunda kutoka katika mti huo, basi nikala.” **13** Ndipo Yehova Mungu akamuuliza mwanamke: “Ni jambo gani hili ulilofanya?” Mwanamke akajibu: “Nyoka alinidanganya, basi nikala.”^c

14 Kisha Yehova Mungu akamwambia nyoka:^d “Kwa sababu umefanya jambo hili, wewe umelaaniwa kati ya wanyama wote wa kufugwa na kati ya wanyama wote wa mwituni. Utakwenda kwa tumbo lako, nawe utakula mavumbi sikuzote za maisha yako. **15** Nami nitaweka uadui^e kati yako^f na mwanamke^g na kati ya uzao wako^h na uzao wake.ⁱ Yeye atakupondaⁱⁱ kichwa,^j nawe utamuumaⁱⁱⁱ kisigino.”^k

16 Akamwambia mwanamke: “Nitazidisha sana uchungu wa mimba yako; utazaa watoto kwa uchungu, nawe

3:15 *Au “uhasama.” ^aTnn., “mbegu yako.” ^bTnn., “mbegu yake.” ^cAu “atakujeruhi; atakugonga.” ^dAu “utamjeruhi; utamponda.”

SURA YA 3

a Mwa 2:25

b Mwa 2:17

c 2Ko 11:3
1Ti 2:14

d Mwa 3:1

e Ufu 12:7,17

f Ufu 12:9

g Ufu 12:1

h Yoh 8:44
1Yo 3:10i Mwa 22:18
Mwa 49:10
Gal 3:16, 29

j Ufu 20:2,10

k Mt 27:50
Mdo 3:15

Safu ya 2

a Mwa 2:17

b Mwa 5:29

c Ro 8:20

d Mwa 2:7

e Zb 104:29
Mhu 3:20
Mhu 12:7

f Mdo 17:26

g Mwa 3:7

h Mwa 3:5

i Mwa 2:9

j Mwa 2:8

k Mwa 3:19

l Zb 80:1
Isa 37:16
Eze 10:4

utamtamani sana mume wako, naye atakutawala.”

17 Kisha akamwambia Adamu:^{*} “Kwa sababu uliisikiliza sauti ya mke wako na kula matunda ya mti ambao nilikuamuru^a hivi kuuhusu, ‘Usile matunda yake,’ ardhi imelaaniwa kwa sababu yako.^b Kwa maumivu utakula mazao yake sikuzote za maisha yako.^c **18** Itakuzalia miiba na michongoma, nawe utakula mimea ya shambani. **19** Kwa jasho la uso wako utakula chakula^{*} mpaka utakaporudi ardhi, kwa kuwa ulitolewa humo.^d Kwa maana wewe ni mavumbi nawe utarudi mavumbini.”^e

20 Baada ya hayo Adamu akampa mke wake jina Hawa,^{*} kwa sababu angekuwa mama ya kila mtu anayeishi.^f **21** Na Yehova Mungu akamtengenezea Adamu na mke wake mavazi marefu ya ngozi ili wavae.^g **22** Kisha Yehova Mungu akasema: “Tazama mtu huyu amekuwa kama sisi kwa kujua mema na mabaya.^h Sasa ili asiunyooshe mkono wake na kuchukua pia matunda kutoka katika mti wa uzima,ⁱ naye ale na kuishi milele,—” **23** Ndipo Yehova Mungu akamfukuza kutoka katika bustani ya Eden^j ili ailime ardhi ambamo alikuwa ametolewa.^k **24** Basi akamfukuza mtu huyo, akaweka upande wa mashariki wa bustani ya Eden^j makerubi^l na upanga unaowaka uliokuwa ukizunguka mfululizo ili kuilinda njia ya kwenda kwenye mti wa uzima.

3:17 *Maana yake “Mtu wa Udongo; Binadamu; Mwanadamu.” 3:19 *Tnn., “mkate.” 3:20 *Maana yake “Anayeishi.”

4 Basi Adamu akafanya ngono na Hawa mke wake, na Hawa akapata mimba.^a Akamzaa Kaini^b na kusema: “Nimezaa mtoto wa kiume kwa msaada wa Yehova.” **2** Baadaye akamzaa Abeli,^c ndugu ya Kaini.

Abeli akawa mchungaji, lakini Kaini akawa mkulima. **3** Baada ya muda, Kaini alileta baadhi ya mazao ya shambani ili ayatoe kuwa dhabihu kwa Yehova. **4** Lakini Abeli alileta baadhi ya wazaliwa wa kwanza wa mifugo^d yake, pamoja na mafuta yao. Yehova alipendezwa na Abeli na dhabihu^e yake, **5** lakini hakupendezwa hata kidogo na Kaini na dhabihu yake. Basi Kaini akawaka hasira kali na kusononeka.* **6** Basi Yehova akamuuliza Kaini: “Kwa nini umekasirika sana na kusononeka? **7** Ukitenda mema, je, hutapata kibali tena?” Lakini usipotenda mema, dhabhi inakunyemelea mlangoni, nayo inatamani sana kukutawala; lakini je, utaihinda?”

8 Baada ya hayo Kaini akamwambia Abeli ndugu yake: “Twende zetu shambani.” Basi walipokuwa shambani, Kaini akamshambulia Abeli ndugu yake, akamuua.^f **9** Baadaye, Yehova akamuuliza Kaini: “Yuko wapi Abeli ndugu yako?” naye akajibu: “Sijui. Kwani mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” **10** Basi Mungu akasema: “Umefanya nini? Sikiliza! Damu ya ndugu yako inanililia kwa sauti kutoka ardhini.^g **11** Na sasa ume-laaniwa kwa kufukuzwa kuto-

4:5 *Tnn., “na uso wake ukakunjamana.”
4:7 *Au “hutakwezwa?”

SURA YA 4

a Mwa 1:28

b IYo 3:10-12
Yud 11

c Mt 23:35

d Kut 13:12

e Ebr 11:4

f Mt 23:35
IYo 3:10-12
Yud 11

g Ebr 12:24

Safu ya 2

a Mwa 9:5

b Mwa 2:8

c Mwa 5:4

ka katika ardhi ambayo imefungua kinywa chake ili kupokea damu ya ndugu yako kutoka mkononi mwako.^a

12 Utakapolima ardhi, haitakurudishia mazao yake.* Utakuwa mtu anayetangatanga na mkimbizi duniani.” **13** Kisha Kaini akamwambia Yehova: “Adhabu ya kosa langu ni kubwa mno kwangu kustahimili. **14** Leo unanifukuza kutoka katika nchi hii,* nami nitafichwa kutoka mbele za uso wako; nitakuwa mtu anayetangatanga na mkimbizi duniani, na yeyote atakayenipata kwa hakika ataniua.” **15** Kwa hiyo Yehova akamwambia: “Kwa sababu hiyo, yeyote atakayemuua Kaini atalipizwa kisasi mara saba.”

Basi Yehova akaweka alama kwa ajili ya Kaini ili yeyote atakayempata asimue. **16** Kisha Kaini akaenda zake kutoka mbele za Yehova, akaanza kuishi katika nchi ya Uhamisho,* upande wa mashariki wa Edeni.^b

17 Baadaye Kaini akafanya ngono na mke wake,^c naye akapata mimba na kumzaa Enoko. Kisha akajenga jiji na kuliita jiji hilo Enoko, jina la mwanawe. **18** Baadaye Enoko akamzaa Iradi. Na Iradi akamzaa Mehuyaeli, na Mehuyaeli akamzaa Methushaeli, na Methushaeli akamzaa Lameki.

19 Lameki akaoa wake wawili. Mke wa kwanza aliitwa Ada, na wa pili aliitwa Zila. **20** Ada akamzaa Yabali. Ndiye aliyekuwa mwanzil-

4:12 *Tnn., “nguvu zake.” 4:14 *Tnn., “kutoka kwenye uso wa ardhi.” 4:16 *Au “nchi ya Nodi.”

lishi wa wale wanaokaa kati-ka mahema na wenye mifugo. **21** Ndugu yake aliitwa Yubali. Ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa wale wote wanaopiga kinubi na zumari.* **22** Pia Zila alimzaa Tubal-kaini, aliyekuwa akitengeneza vifaa vya kila aina vya shaba na chuma. Na dada ya Tubal-kaini aliitwa Naama. **23** Kisha Lameki akatunga maneno haya kwa ajili ya wake zake, Ada na Zila:

“Sikieni sauti yangu, enyi wake za Lameki;

Sikilizeni maneno yangu: Nimemuua mwanamume kwa sababu ya kunijeruhi,

Naam, mwanamume kijana kwa sababu ya kunipiga.

24 Ikiwa Kaini atalipizwa kisasi mara 7,^a

Basi Lameki ni mara 77.”

25 Adamu akafanya ngona tena na mke wake, naye akazaa mwana. Akampa jina Sethi,^{*b} kwa sababu kama mama yake alivyosema, “Mungu amenichagulia mzao mwingine” atakayechukua mahali pa Abeli, kwa sababu Kaini alimuua.”^c **26** Pia Sethi akazaa mwana na kumpa jina Enoshi.^d Wakati huo watu walianza kuliitia jina la Yehova.

5 Hiki ndicho kitabu cha historia ya Adamu. Siku ambayo Mungu alimuumba Adamu, alimuumba kwa mfanano wa Mungu.^e **2** Mwanamume na mwanamke aliwauumba.^f Siku ambayo aliwauumba,^g aliwabariki na kuwaita Binadamu.*

4:21 *Au “filimbi.” 4:25 *Maana yake “Aliyechaguliwa; Aliyesimamishwa.”^a *Tnn., “mbegu nyingine.” 5:2 *Au “Adamu; Wanadamu.”

SURA YA 4

a Mwa 4:15

b Mwa 5:3
1Nya 1:1c Mwa 4:8
Mt 23:35
Ebr 11:4d Mwa 5:6
Lu 3:23, 38

SURA YA 5

e Mwa 1:26
Yak 3:9f Mwa 1:27
Mk 10:6g Mwa 2:23
Isa 45:12
Mt 19:4

Safu ya 2

a Mwa 4:25

b Mwa 2:17
Mwa 3:19
Ro 6:23
1Ko 15:22c Mwa 4:26
Lu 3:23, 38

d Lu 3:23, 37

e Lu 3:23, 37

f Yud 14

g Lu 3:23, 37

3 Adamu aliishi miaka 130, kisha akazaa mwana kwa mfanano wake, kwa sura yake, akampa jina Sethi.^a **4** Baada ya kumzaa Sethi, Adamu aliishi miaka 800. Naye akazaa wana na mabinti. **5** Basi siku zote za maisha ya Adamu zilikuwa miaka 930, kisha akafa.^b

6 Sethi aliishi miaka 105, akamzaa Enoshi.^c **7** Baada ya kumzaa Enoshi, Sethi aliishi miaka 807. Naye akazaa wana na mabinti. **8** Basi siku zote za maisha ya Sethi zilikuwa miaka 912, kisha akafa.

9 Enoshi aliishi miaka 90, kisha akamzaa Kenani. **10** Baada ya kumzaa Kenani, Enoshi aliishi miaka 815. Naye akazaa wana na mabinti. **11** Basi siku zote za maisha ya Enoshi zilikuwa miaka 905, kisha akafa.

12 Kenani aliishi miaka 70, kisha akamzaa Mahalaleli.^d

13 Baada ya kumzaa Mahalaleli, Kenani aliishi miaka 840. Naye akazaa wana na mabinti. **14** Basi siku zote za maisha ya Kenani zilikuwa miaka 910, kisha akafa.

15 Mahalaleli aliishi miaka 65, kisha akamzaa Yaredi.^e

16 Baada ya kumzaa Yaredi, Mahalaleli aliishi miaka 830. Naye akazaa wana na mabinti. **17** Basi siku zote za maisha ya Mahalaleli zilikuwa miaka 895, kisha akafa.

18 Yaredi aliishi miaka 162, kisha akamzaa Enoko.^f

19 Baada ya kumzaa Enoko, Yaredi aliishi miaka 800. Naye akazaa wana na mabinti.

20 Basi siku zote za maisha ya Yaredi zilikuwa miaka 962, kisha akafa.

21 Enoko aliishi miaka 65, kisha akamzaa Methusela.^g

22 Baada ya kumzaa Methusela, Enoko aliendelea kutembea na Mungu wa kweli kwa miaka 300. Naye akazaa wana na mabinti. **23** Basi siku zote za maisha ya Enoko zilikuwa miaka 365. **24** Enoko aliendelea kutembea na Mungu wa kweli.^a Kisha hakuwepo tena, kwa maana Mungu alimchukua.^b

25 Methusela aliishi miaka 187, kisha akamzaa Lameki.^c **26** Baada ya kumzaa Lameki, Methusela aliishi miaka 782. Naye akazaa wana na mabinti. **27** Basi siku zote za maisha ya Methusela zilikuwa miaka 969, kisha akafa.

28 Lameki aliishi miaka 182, kisha akazaa mwana. **29** Akamwita mwana huyo Noa,^{*d} akisema: "Huyu atafuriji katika kazi yetu ngumu na katika kazi inayomiza ya mikono yetu kwa sababu ya ardhi iliyolaaniwa^e na Yehova." **30** Baada ya kumzaa Noa, Lameki aliishi miaka 595. Naye akazaa wana na mabinti. **31** Basi siku zote za maisha ya Lameki zilikuwa miaka 777, kisha akafa.

32 Baada ya Noa kuishi miaka 500, alimzaa Shemu,^f Hamu,^g na Yafethi.^h

6 Sasa idadi ya wanadamu ilipoanza kuongezeka duniani, nao wakazaa mabinti, 2 wana wa Mungu wa kweli^{*i} wakaanza kuona kwamba mabinti wa wanadamu ni warembo. Basi wakaanza kuwachukua wote waliowachagua ili wawe wake zao.

5:29 *Huenda jina hili linamaanisha "Pumzikio; Faraja." 6:2 *Msemo wa Kiberania unaorejelea malaika, wana wa Mungu.

SURA YA 5

a Mwa 6:9
Kum 8:6
Kum 13:4
3Yo 4
Yud 14, 15

b Yoh 3:13
Ebr 11:5

c Lu 3:23, 36

d Mwa 7:1
Eze 14:14
Mt 24:37
Ebr 11:7
1Pe 3:20
2Pe 2:5

e Mwa 3:17

f Mwa 10:21
Mwa 11:10
Lu 3:23, 36

g Mwa 6:10
Mwa 10:6

h Mwa 10:2

SURA YA 6

i Ayu 1:6
Ayu 38:7
2Pe 2:4
Yud 6

Safu ya 2

a Mwa 7:4
1Pe 3:20

b 2Pe 3:9

c Mwa 8:21
Yer 17:9
Mt 15:19

d Zb 78:40, 41

e Mwa 7:1
Eze 14:14
Ebr 11:7

f 2Pe 2:5

3 Ndipo Yehova akasema: "Roho yangu haitamvumilia mwanadamu daima,^a kwa sababu yeye ni mwili tu.* Kwa hiyo, jumla ya siku zake itakuwa miaka 120."^b

4 Wanefili* walikuwa duniani siku hizo na baadaye. Wakati huo wana wa Mungu wa kweli waliendelea kufanya ngono na mabinti wa wanadamu, nao wakawazalia wana. Wana hao walikuwa watu wenye nguvu wa nyakati za kale, wanaume maarufu.

5 Basi, Yehova akaona kwamba uovu wa mwanadamu ulikuwa mkubwa duniani na kwamba kila mwelekeo wa mawazo ya moyo wake ulikuwa mbaya tu wakati wote.^c

6 Yehova akaghairi* kwamba aliwaumba wanadamu duniani, na moyo wake ukahuzunika.^{*d} **7** Kwa hiyo Yehova akasema: "Nitawafagilia mbali kutoka duniani wanadamu ambao nimewaumba, wanadamu pamoja na wanyama wa kufugwa, wanyama wanaotamba, na viumbe wanaoruka angani, kwa sababu ninaghairi kwamba niliwaumba." **8** Lakini Noa akapata kibali machoni pa Yehova.

9 Hii ndiyo historia ya Noa. Noa alikuwa mtu mwadilifu.^e Alijithibitisha mwenyewe kuwa mtu asiye na kosa* miongoni mwa watu wa siku zake.^{*f} Noa alitembea pamoja na Mungu wa kweli.^f

6:3 *Au "kwa sababu anatenda kulingana na mwili." 6:4 *Huenda neno hili linamaanisha "Waangushaji," yaani, wale wanaoangusha wengine chini. Angalia Kamusi, uku. 2012. 6:6 *Au "akasi-kitika." *Au "naye akaumia moyoni mwake." 6:9 *Au "lawama." *Tnn., "vizazi vyake."

10 Baada ya muda, Noa alizaa wana watatu, Shemu, Hamu, na Yafethi.^a **11** Lakini dunia ilikuwa imeharibika machoni pa Mungu wa kweli, nayo dunia ilikuwa imejaa ukatili. **12** Naam, Mungu alitazama dunia, nayo ilikuwa imeharibika;^b watu wote walikuwa wameharibu njia yao duniani.^c

13 Baada ya hayo Mungu akamwambia Noa: "Nimeama kuwaangamiza wanadamu wote, kwa sababu wamejaza dunia ukatili, kwa hiyo nitawaangamiza pamoja na dunia.^d **14** Jitengenezee safina* kwa mbao za mti wenye utomvu.^e Utatengeneza vyumba ndani ya safina na uifunike kwa lami^f ndani na nje. **15** Hivi ndivyo utakavyoitengeneza: Safina inapaswa kuwa na urefu wa mikono 300,* upana wa mikono 50, na kimo cha mikono 30. **16** Utatengeneza dirisha la kuingiza mwangaza kwenye safina,* mkono mmoja kutoka juu. Unapaswa kutengeneza mlango ubavuni mwake,^g na utengeneze ghorofa ya chini, ghorofa ya pili, na ghorofa ya tatu.

17 "Nami kwa upande wangu, nitaleta gharika ya maji^h duniani ili kuangamiza viumbe wote wenye pumzi ya uhai* walio chini ya mbingu. Kila kitu kilicho duniani kitaangamia.ⁱ **18** Nami ni-

6:14 *Tnn., "sanduku"; chombo kiku-bwa. **6:15** *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. **6:16** *Katika Kiebrania ni tso'har. Baadhi ya watu wanasema kwamba tso'har ni nafasi ya mkono mmoja kati ya paa na dari, si dirisha au nafasi ya kuingizia mwangaza. **6:17** *Au "roho ya uhai."

SURA YA 6

a Mwa 5:32

b Ufu 11:18

c Mt 24:37-39
2Pe 2:5

d Mwa 7:4

e Ebr 11:7

f Mwa 14:10
Kut 2:3

g Mwa 7:16

h Mwa 1:7
Mwa 7:6, 11i Mwa 7:21
Zb 104:29
Mt 24:39
2Pe 2:5

Safu ya 2

a Mwa 7:13

b Mwa 8:17

c Mwa 7:2

d Mwa 7:14, 15

e Mwa 1:29, 30

f Kut 40:16
Ebr 11:7

SURA YA 7

g Mwa 6:9
Ebr 10:38
Ebr 11:7
1Pe 3:12
2Pe 2:5, 9

h Mwa 8:20

i Mwa 7:23
Mwa 8:19

j Mwa 2:5

k Mwa 7:11, 12

nafanya pamoja nawe agano langu, nawe lazima uingie ndani ya safina, wewe, wanao, mke wako, na wake wa wanao.^a **19** Nawe uingize ndani ya safina viumbe hai^b wawili wawili wa kila aina ili kuwahifadhi hai pamoja nawe, dume na jike;^c **20** viumbe wanaoruka angani kulingana na aina zao, wanyama wa kufugwa kulingana na aina zao, na wanyama wote wanaotambaa kulingana na aina zao, watakuja ndani kwako viumbe wawili wawili wa kila aina ili uwahifadhi hai.^d **21** Nawe unapaswa kukusanya na kuchukua kila aina ya chakula,^e kwa ajili yako na wanyama.^f

22 Basi Noa akafanya kulingana na mambo yote ambayo Mungu alikuwa amemwamuru. Hivyo ndivyo alivyofanya.^f

7 Baada ya hayo Yehova akamwambia Noa: "Ingia ndani ya safina, wewe pamoja na watu wote wa nyumbani mwako, kwa sababu nimekuona wewe peke yako kuwa mwadilifu mbele zangu miongoni mwa kizazi hiki.^g **2** Ingia pamoja na wanyama safi wa kila aina, saba saba,^{*h} dume na jike; na wanyama wawili tu wasio safi wa kila aina, dume na jike; **3** pia viumbe wanaoruka angani saba saba,* dume na jike, ili kuhifadhi hai uzao wao duniani pote.ⁱ **4** Kwa maana baada ya siku saba tu, nitafanya mvua inyeshe^j duniani siku 40 mchana na usiku,^k nami nitafagilia mbali kutoka duniani kila kiumbe kilicho hai

7:2 *Au labda, "jozi saba za kila mnyama aliye safi." **7:3** *Au labda, "jozi saba za viumbe wanaoruka angani."

nilichokiumba.”^a **5** Basi Noa akafanya yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru.

6 Noa alikuwa na umri wa miaka 600 maji ya gharika yalipokuja duniani.^b **7** Kwa hiyo Noa, pamoja na wanawe, mke wake, na wake wa wanawe, wakaingia ndani ya safina kabla ya maji ya gharika kuja.^c

8 Kila aina ya mnyama aliye safi na kila aina ya mnyama asiye safi na kila aina ya kiumbe anayeruka angani na kila aina ya kiumbe anayetambaa ardhini,^d **9** wakaingia wawili wawili na kumjia Noa ndani ya safina, dume na jike, kama Mungu alivyokuwa amemwamuru Noa. **10** Na siku saba baadaye maji ya gharika yaka-ja duniani.

11 Katika mwaka wa 600 wa maisha ya Noa, mwezi wa pili, siku ya 17 ya mwezi huo, siku hiyo chemchemi zote za kilindi kikubwa cha maji zili-funguka kwa nguvu na malango ya mbinguni ya mafuriko yakafunguliwa.^e **12** Na mvua ikamwagika duniani kwa siku 40, mchana na usiku. **13** Siku hiyohiyo, Noa aliingia ndani ya safina pamoja na wanawe, Shemu, Hamu, na Yafethi,^f pamoja na mke wake na wake watatu wa wanawe.^g **14** Waliingia ndani pamoja na kila mnyama wa mwituni kulingana na aina yake, na kila mnyama wa kufugwa kulingana na aina yake, na kila mnyama anayetambaa duniani kulingana na aina yake, na kila kiumbe anayeruka kulingana na aina yake, kila ndege, kila kiumbe mwenye mabawa. **15** Waliendelea kumjia Noa ndani ya safina, wawili wawili,

SURA YA 7

- a Mwa 6:7,17
 - b Mwa 8:13
 - c Lu 17:27
Ebr 11:7
 - d Mwa 6:19, 20
 - e Mwa 1:7
Mwa 8:2
 - f Mwa 9:18
1Nya 1:4
 - g Mwa 6:18
1Pe 3:20
2Pe 2:5
- Safu ya 2
- a 2Pe 3:5, 6
 - b Mwa 6:7,17
 - c Lu 17:27
 - d Mwa 2:7
Mwa 7:15
Mhu 3:19
Isa 42:5
 - e Mwa 6:7
2Pe 3:5, 6
 - f Mt 24:37-39
1Pe 3:20
2Pe 2:5, 9
 - g Mwa 8:3

kila aina ya kiumbe mwenye pumzi ya uhai.* **16** Basi wakaingia ndani, dume na jike, viumbe wa kila aina, kama Mungu alivyokuwa amemwamuru. Baada ya hayo Yehova akaufunga mlango.

17 Gharika ikaendelea* kwa siku 40 duniani, na maji yakazidi kuongezeka, yakaa-nza kuibeba safina, nayo safina ikaelea juu sana duniani. **18** Maji yakafurika na kuzidi kuongezeka sana duniani, lakini safina ilielea juu ya maji. **19** Maji yalifurika sana duniani hivi kwamba milima yote mirefu chini ya mbingu ikafunikwa.^a **20** Maji yalipanda kufikia mikono 15* juu ya milima.

21 Basi viumbe wote walio hai waliotembea duniani wakafa^b—viumbe wanaoruka, wanyama wa kufugwa, wanyama wa mwituni, viumbe wanaoishi katika makundi makubwa, na wanadamu wote.^c **22** Kila kiumbe katika nchi kavu aliyekuwa na pumzi ya uhai* katika mianzi ya pua yake akafa.^d **23** Basi Mungu akafagilia mbali kila kiumbe hai kutoka duniani, kutia ndani, wanadamu, wanyama, wanyama wanaotambaa, na viumbe wanaoruka angani. Wote walifagiliwa mbali kutoka duniani;^e ni Noa peke yake na wale waliokuwa pamoja naye ndani ya safina waliookoka.^f **24** Na maji yakaendelea kufunika dunia kwa siku 150.^g

7:15 *Au “roho ya uhai.” 7:17 *Au “ikaendelea kumwagika.” 7:20 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. 7:22 *Au “pumzi ya roho ya uhai.”

8 Lakini Mungu akamwelekeza uangalifu* Noa na wanyama wote wa mwituni na wanyama wa kufugwa walio-kuwa pamoja naye ndani ya safina,^a na Mungu akavumisha upepo duniani, maji yakaanza kupungua. **2** Chemchemi za kilindi cha maji na malango ya mbinguni ya mafuriko yakafungwa, kwa hiyo mvua kutoka mbinguni ikaacha kunyesha.*^b **3** Kisha maji yakaanza kupungua hatua kwa hatua duniani. Kufikia mwishoni mwa siku 150, maji yalikuwa yamepungua sana. **4** Katika mwezi wa saba, siku ya 17 ya mwezi huo, safina ikatua kwenye milima ya Ararati. **5** Na maji yakazidi kupungua hatua kwa hatua mpaka mwezi wa kumi. Katika mwezi wa kumi, siku ya kwanza ya mwezi huo, vilele vya milima vikaonekana.^c

6 Basi mwishoni mwa siku 40, Noa akafungua dirisha^d la safina alilokuwa ametengeneza **7** na kumtuma nje kunguru; kunguru alikuwa akienda na kurudi, mpaka maji yalipokauka duniani.

8 Baadaye akamtuma njiwa ili aone ikiwa maji yalikuwa yamepungua ardhini. **9** Njiwa huyo hakupata mahali pa kutua,* kwa hiyo akarudi kwa Noa ndani ya safina kwa saba- bu maji yalikuwa bado yameifunika dunia yote.^e Kwa hiyo akaunyoosha mkono wake nje na kumwingiza ndani ya safina. **10** Noa akangojewa siku saba zaidi, akamtuma tena njiwa nje ya safina. **11** Njiwa

8:1 *Tnn., "akamkumbuka." 8:2 *Au "ikazuliwa." 8:9 *Au "mahali pa kutua kwa ajili ya wayo wa mguu wake."

SURA YA 8

a Mwa 6:19, 20
Ebr 11:7

b Mwa 7:11, 12

c Mwa 7:20

d Mwa 6:16

e Mwa 7:19

Safu ya 2

a Mwa 7:20
Mwa 8:3

b Mwa 7:6, 11

c Mwa 7:7
Ipe 3:20
ZPe 2:5

d Mwa 6:19, 20
Mwa 7:14, 15

e Mwa 1:22

f Mwa 6:10

g Mwa 7:13, 14

h Mwa 12:7

i Mwa 7:2
Law 20:25

j Kum 27:6

huyo alipomrudia Noa ikielekea jioni, aliona kwamba alikuwa na jani bichi la mzeituni mdomoni mwake! Basi Noa akajua kwamba maji yalikuwa yamepungua duniani.^a **12** Akangojewa tena siku nyi-ngine saba. Kisha akamtuma nje njiwa huyo, lakini hakurudi tena.

13 Sasa katika mwaka wa 601,^b mwezi wa kwanza, siku ya kwanza ya mwezi huo, maji yalikuwa yamepungua duniani; Noa akaondoa kifuniko cha safina na kuona kwamba ardhi ilikuwa ikikauka. **14** Katika mwezi wa pili, siku ya 27 ya mwezi huo, dunia ilikuwa imekauka.

15 Sasa Mungu akamwambia Noa: **16** "Toka ndani ya safina, wewe, mke wako, wanao, na wake zao."^c **17** Toka pamoja na viumbe wote walio hai wa kila aina,^d viumbe wanaoruka, wanyama, na wanyama wote wanaotambaa, ili wazaane* duniani na kuongezeka na kuwa wengi duniani."^e

18 Basi Noa akatoka nje, pamoja na wanawe,^f mke wake, na wake wa wanawe. **19** Kila kiumbe aliye hai, kila mnyama anayetambaa na kila kiumbe anayeruka, kila kiumbe anayetembea duniani, akatoka ndani ya safina kulingana na familia yake.^g **20** Kisha Noa akamjengea Yehova madhabahu,^h akachukua baadhi ya wanyama walio safi na baadhi ya viumbe wanaoruka walio safi,ⁱ akawatoa kuwa dhabihu za kuteketezwa juu ya madhabahu/hiyo. **21** Na Yehova akaanza

8:17 *Au "wajae."

kusikia harufu ya kupendeza.* Kwa hiyo Yehova akasema moyoni mwake: “Sitailaani ardhia tena kwa sababu ya mwanadamu, kwa maana mwelekeo wa moyo wa mwanadamu ni mbaya tangu wakati wa ujana;^b nami sitamwangamiza tena kamwe kila kiumbe aliye hai kama nilivyofanya.^c **22** Kuanzia sasa na kuendelea, dunia haitakosa kamwe kuwa na majira ya kupanda mbevu na kuvuna, baridi na joto, kiangazi na masika, na mchana na usiku.”^d

9 Basi Mungu akambariki Noa na wanawe na kuwambia: “Zaeni muwe wengi na kuijaza dunia.^e **2** Kila kiumbe aliye hai duniani na kila kiumbe anayeruka angani na kila kiumbe anayetambaa ardhini na samaki wote wa baharini wataendelea kuwaogopa na kuwahofu ninyi. Sasa nimewatia mikononi mwenu.*^f **3** Kila mnyama aliye hai anayetembea anaweza kuwa chakula chenu.^g Kama nilivyowapa mimea, ninawapa hao wote wawe chakula chenu.^h **4** Ila tu nyama pamoja na uhai wake*—damu yakeⁱ—hampaswi kula.^j **5** Zaidi ya hayo, nitadai muwajibike kwa sababu ya damu ya uhai wenu.* Nitadai kila kiumbe aliye hai awajibike; nami nitamdai kila mwanadamu awajibike kwa sababu ya uhai wa ndugu yake.^k **6** Yeyote anayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake mwenyewe itamwaga^l na mwanadamu, kwa maana

8:21 *Au “inayotuliza.” 9:2 *Au “nime-waweka chini ya mamlaka yenu.” 9:4 *Au “nafsi yake.” 9:5 *Au “damu ya nafsi zenu.”

SURA YA 8

a Mwa 3:17
Mwa 5:29

b Mwa 6:5
Mhu 7:20
Mt 15:19

c Mwa 6:7,17
Mwa 9:11
Isa 54:9

d Mwa 1:14
Zb 74:17
Mhu 1:4

SURA YA 9

e Mwa 1:28

f Mwa 1:26
Yak 3:7

g ITi 4:3

h Mwa 1:29

i Law 17:11, 14

j Law 3:17
Law 7:26
Law 17:10, 13
Kum 12:16, 23
Mdo 15:20, 29
Mdo 21:25

k Mwa 4:8, 10
Kut 21:12

l Kut 20:13
Hes 35:30
Mt 26:52

Safu ya 2

a Mwa 1:27

b Mwa 1:28
Mwa 10:32

c Mwa 9:15
Isa 54:9

d Mwa 8:17

e Mwa 8:21

f Mwa 8:21

Mungu alimuumba mwanadamu^a kwa mfano Wake. **7** Lakini ninyi, zaeni muwe wengi, mwongezeke kwa wingi na kujaa^b duniani.”

8 Kisha Mungu akamwambia Noa na wanawe: **9** “Sasa ninafanya agano langu pamoja nanyi^c na pamoja na wazao wenu baada yenu, **10** na pamoja na kila kiumbe aliye hai ambaye yupo* pamoja nanyi, ndege, wanyama, na viumbe wote walio hai duniani pamoja nanyi, wote waliotoka ndani ya safina—kila kiumbe aliye hai duniani.^d **11** Naam, ninafanya agano langu pamoja nanyi: Viumbe wote* hawataangamizwa tena kamwe kwa maji ya gharika, na gharika haitaiharibu^e dunia tena kamwe.”

12 Na Mungu akaendelea kusema: “Hii ndiyo ishara ya agano ninalofanya pamoja nanyi na pamoja na kila kiumbe hai aliye pamoja nanyi, kwa vizazi vyote vijavyo. **13** Ninauweka upinde wangu wa mvua mawinguni, nao utakuwa ishara ya agano nililofanya na dunia. **14** Kila mara ninaoleta mawingu juu ya dunia, kwa hakika upinde wa mvua utaonekana mawinguni. **15** Nami hakika nitakumbuka agano langu nililofanya pamoja nanyi na pamoja na kila aina ya kiumbe aliye hai; na kamwe hakutakuwa tena na gharika ya maji itakayowaangamiza viumbe wote.^f **16** Na upinde wa mvua utatokea mawinguni, nami hakika nitauona na kukumbuka agano la milele ambalo mimi Mu-

9:10 *Au “nafsi iliyo hai iliyo.” 9:11 *Au “Viumbe wote walio hai.”

ngu nilifanya pamoja na kila aina ya kiumbe hai duniani.”

17 Mungu akarudia kumwambia Noa: “Hii ndiyo ishara ya agano ninalofanya pamoja na viumbe wote walio duniani.”^a

18 Hawa ndio wana wa Noa waliotoka ndani ya safina: Shemu, Hamu, na Yafethi.^b Baadaye Hamu akamzaa Kanaani.^c **19** Hao watatu walikuwa wana wa Noa, na watu wote duniani walitokana nao na kuenea kotekote.^d

20 Sasa Noa akaanza kuli- ma, akapanda shamba la mizabibu. **21** Alipokunywa divai, alilewa, naye akavua nguo ndani ya hema lake. **22** Hamu, baba ya Kanaani, akamwona baba yake akiwa uchi, akawaambia ndugu zake wawili waliokuwa nje. **23** Kwa hiyo Shemu na Yafethi wakachukua nguo na kuiweka mabegani mwao na kuingia ndani kinyumenyume. Basi wakaufunika uchi wa baba yao huku nyuso zao zikitazama pembeni, nao hawakuuona uchi wa baba yao.

24 Divai ilipomtoka Noa, naye akasikia jambo ambalo mwanawe mdogo alimtendea, **25** akasema:

“Alaaniwe Kanaani.^e

Na awe mtumwa wa hali ya chini kabisa kwa ndugu zake.”^f

26 Pia akasema:

“Asifiwe Yehova, Mungu wa Shemu, Acha Kanaani awe mtumwa wake.”^g

27 Mungu na ampe Yafethi nafasi ya kutosha, Na akae katika mahema ya Shemu.

SURA YA 9

a Mwa 9:12, 13

b Mwa 5:32
Mwa 7:7
Mwa 10:1

c Mwa 10:6

d Mwa 10:32

e Kum 7:1

f Yos 17:13

g Amu 1:28

Safu ya 2

a Mwa 7:6

SURA YA 10

b Lu 3:23, 36

c Mwa 9:18, 19

d Eze 38:6

e Eze 38:2

f Isa 66:19
Eze 27:13

g Zb 120:5
Eze 32:26

h 1Nya 1:5-7

i Yer 51:27

j Eze 27:14
Eze 38:6

k Eze 27:7

l Yon 1:3

m Isa 23:1

n Mwa 50:11

o Yer 46:9
Nah 3:9

p Hes 34:2
1Nya 1:8-10

q Zb 72:10

r Eze 27:22

s Mwa 11:9

t Eze 4:9

u Da 1:2

Kanaani na awe mtumwa wake pia.”

28 Noa akaendelea kuishi miaka 350 baada ya Gharika.^a

29 Basi siku zote za maisha ya Noa zilikuwa miaka 950, kisha akafa.

10 Hii ndiyo historia ya wana wa Noa, yaani, Shemu,^b Hamu, na Yafethi.

Walizaa wana baada ya Gharika.^c **2** Wana wa Yafethi walikuwa Gomeri,^d Magogu,^e Madai, Yavani, Tubali,^f Mesheki,^g na Tirasi.^h

3 Wana wa Gomeri walikuwa Ashkenazi,ⁱ Rifathi, na Togarma.^j

4 Wana wa Yavani walikuwa Elisha,^k Tarshishi,^l Kitiimu,^m na Dodanimu.

5 Kutokana na hawa, wakaa-ji wa visiwani walienea katika nchi zao, kulingana na lugha zao na koo zao na kulingana na mataifa yao.

6 Wana wa Hamu walikuwa Kushi, Misraimu,ⁿ Putu,^o na Kanaani.^p

7 Wana wa Kushi walikuwa Seba,^q Havila, Sabta, Raama,^r na Sabteka.

Wana wa Raama walikuwa Sheba na Dedani.

8 Kushi akamzaa Nimrodi. Nimrodi ndiye aliye-kuwa shujaa wa kwanza duniani. **9** Alikuwa mwindaji hodari aliyempinga Yehova. Ndiyo sababu kuna msemo usemao: “Kama Nimrodi, mwindaji hodari aliye-mpinga Yehova.” **10** Ufalme wake ulianza* Babeli,^s Ereki,^t Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari.^u

10:10 * Au “Majiji ya kwanza ya ufalme wake yalikuwa.”

11 Kutoka katika nchi hiyo alienda Ashuru^a na kujenga Ninawi,^b Rehoboth-Iri, Kala, **12** na Reseni, kati ya Ninawi na Kala: Hilo ndilo lile jiji kubwa.*

13 Misraimu akamzaa Ludimu,^c Anamimu, Lehabimu, Naftuhimu,^d **14** Pathrusimu,^e Kasluhimu (hao ndio waliowazaa Wafilisti),^f na Kaftorimu.^g

15 Kanaani akamzaa Sidoni,^h mzaliwa wake wa kwanza, na Hethi,ⁱ **16** na pia Wayebusi,^j Waamori,^k Wagirgashi, **17** Wahivi,^l Waarkia, Wasini, **18** Waarvadi,^m Wasemari, na Wahamathi.ⁿ Baadaye, koo za Wakanaani zilitawanyika. **19** Basi mpaka wa Wakanaani ulianzia Sidoni mpaka Gerari,^o karibu na Gaza,^p hadi Sodoma, Gomora,^q Adma, na Seboiimu,^r karibu na Lasha. **20** Hao ndio waliokuwa wana wa Hamu kulingana na koo zao, lugha zao, nchi zao, na mataifa yao.

21 Shemu, babu ya wana wote wa Eberi^s na ndugu ya Yafethi mkubwa kuliko wote,* pia alizaa watoto. **22** Wana wa Shemu walikuwa Elamu,^t Asihuru,^u Arpakshadi,^v Ludi, na Aramu.^w

23 Wana wa Aramu walikuwa Usi, Huli, Getheri, na Mashi.

24 Arpakshadi akamzaa Shela,^x naye Shela akamzaa Eberi.

25 Eberi alizaa wana wawili. Mmoja aliitwa Pelegi,^{*y}

10:12 *Au labda, "Yanafanyiza lile jiji kubwa." 10:21 *Au labda, "ndugu mkubwa wa Yafethi." 10:25 *Maana yake "Mgawanyiko."

SURA YA 10

- a Mik 5:6
- b Yon 3:3
Mt 12:41
- c Yer 46:9
- d 1Nya 1:11, 12
- e Eze 29:14
- f Yos 13:2, 3
Yer 47:4
- g Kum 2:23
- h Yos 13:6
Mk 7:24
- i Mwa 25:10
Mwa 27:46
1Nya 1:13-16
- j Amu 1:21
- k Mwa 15:16
Kum 3:8
- l Yos 11:3
- m Eze 27:11
- n 1Fa 8:65
- o Mwa 20:1
- p Yos 15:20, 47
Mdo 8:26
- q Mwa 13:10
Mwa 19:24
Yud 7
- r Kum 29:23
- s Mwa 11:17
- t Eze 4:9
Mdo 2:8, 9
- u Eze 27:23
- v Mwa 11:10
- w 1Nya 1:17
- x Mwa 11:12
Lu 3:23, 35
- y Mwa 11:16

Safu ya 2

- a 1Nya 1:19
- b 1Nya 1:20-23
- c 1Fa 9:28
1Fa 10:11
- d Mwa 10:5
- e Mwa 9:7
Mwa 9:19
Mdo 17:26

SURA YA 11

- f Mwa 10:9, 10
Da 1:2
- g Mwa 9:1

kwa sababu katika siku zake dunia ilikuwa imegawanyika.* Ndugu yake aliitwa Yoktani.^a

26 Yoktani akamzaa Almodadi, Shelefu, Hazarmavethi, Yera,^b **27** Hadoramu, Uzali, Dikla, **28** Obali, Abimaeli, Sheba, **29** Ofiri,^c Havila, na Yobabu; wote hao walikuwa wana wa Yoktani.

30 Nchi walimokaa ilianzia Mesha mpaka Sefari, eneo lenye milima la Mashariki.

31 Hao ndio waliokuwa wana wa Shemu kulingana na koo zao, lugha zao, nchi zao, na mataifa yao.^d

32 Hizo ndizo zilizokuwa familia za wana wa Noa kulingana na koo zao na mataifa yao. Kutokana nao, mataifa yalienea duniani kote baada ya Gharika.^e

11 Sasa dunia yote iliendelea kuwa na lugha moja na maneno yaleyale.* **2** Walipokuwa wakisafiri kuelekea mashariki, waligundua bonde tambarare katika nchi ya Shinari,^f wakaanza kuishi huko. **3** Kisha wakaambiana: "Njoooni! Tufyatue matofali na kuyachoma." Basi wakatamia matofali badala ya mawe, na lami badala ya saruji. **4** Sasa wakasema: "Haya! Na tujijengee jiji na mnara ambao kilele chake kitafika mbinguni, na tujijengee jina maarufu, ili tusitawanyike katika dunia yote."^g

5 Kisha Yehova akashuka ili aone jiji na mnara ambao wanadamu walikuwa wameje-

10:25 *Au "wakaaji wa dunia walikuwa wamegawanyika." 11:1 *Au "msamiati uleule."

nga. **6** Ndipo Yehova akasema: "Tazama! Watu hawa ni kitu kimoja na wanazungumza lugha moja,^a na hili ndilo jambo waliloanza kufanya. Sasa hakuna jambo lolote wanalokusudia kufanya litakalowashinda. **7** Njoooni! Tushuke^b huko na kuvuruga lugha yao ili kila mmoja wao asiitelewe lugha ya mwenzake." **8** Basi Yehova akawatawanya dunia-ni pote^c kutoka huko, na hatua kwa hatua wakaacha kuje-nga jiji hilo. **9** Ndiyo sababu liliitwa Babeli,^{*d} kwa sababu huko ndiko Yehova alikovuruga lugha ya dunia yote, na kutoka huko Yehova aliwatawanya dunia-ni pote.

10 Hii ndiyo historia ya Shemu.^e

Shemu alikuwa na umri wa miaka 100 alipomzaa Arpakshadi^f miaka miwili baada ya Gharika. **11** Baada ya kumzaa Arpakshadi, Shemu aliishi miaka 500. Akazaa wana na mabinti.^g

12 Arpakshadi alipokuwa na umri wa miaka 35, alimzaa Shela.^h **13** Baada ya kumzaa Shela, Arpakshadi aliishi miaka 403. Akazaa wana na mabinti.

14 Shela alipokuwa na umri wa miaka 30, alimzaa Eberi.ⁱ **15** Baada ya kumzaa Eberi, Shela aliishi miaka 403. Akazaa wana na mabinti.

16 Eberi alipokuwa na umri wa miaka 34, alimzaa Pelegi.^j **17** Baada ya kumzaa Pelegi, Eberi aliishi miaka 430. Akazaa wana na mabinti.

18 Pelegi alipokuwa na umri wa miaka 30, alimzaa Reu.^k **19** Baada ya kumzaa

SURA YA 11

a Mwa 11:1

b Mwa 1:26

c Kum 32:8

d Yer 50:1

e Mwa 6:10
Lu 3:23, 36f Mwa 10:22
1Nya 1:17

g Mwa 10:21

h Mwa 10:24
1Nya 1:18
Lu 3:23, 35i Mwa 10:21
1Nya 1:18j Mwa 10:25
1Nya 1:19

k Lu 3:23, 35

Safu ya 2

a Mwa 11:32
Lu 3:23, 34b Mwa 12:7
Mwa 15:1, 6
Mwa 17:5
Yak 2:23

c Yos 24:2

d Mwa 12:4
Mwa 19:1
2Pe 2:7e Mwa 15:7
Ne 9:7

f Mdo 7:4

g Mwa 12:11
Mwa 17:15
Mwa 20:12, 13
1Pe 3:6h Mwa 22:20
Mwa 24:15i Mwa 16:1, 2
Ro 4:19
Ebr 11:11

j Mwa 11:27, 28

k Mwa 10:19

l Mwa 12:4
Mwa 27:42, 43
Mdo 7:2, 4

Reu, Pelegi aliishi miaka 209. Akazaa wana na mabinti.

20 Reu alipokuwa na umri wa miaka 32, alimzaa Serugi. **21** Baada ya kumzaa Serugi, Reu aliishi miaka 207. Akazaa wana na mabinti.

22 Serugi alipokuwa na umri wa miaka 30, alimzaa Nahori. **23** Baada ya kumzaa Nahori, Serugi aliishi miaka 200. Akazaa wana na mabinti.

24 Nahori alipokuwa na umri wa miaka 29, alimzaa Tera.^a **25** Baada ya kumzaa Tera, Nahori aliishi miaka 119. Akazaa wana na mabinti.

26 Tera alipokuwa na umri wa miaka 70, alimzaa Abram,^b Nahori,^c na Harani.

27 Hii ndiyo historia ya Tera.

Tera alimzaa Abram, Nahori, na Harani; naye Harani akamzaa Loti.^d **28** Tera, baba yake, alipokuwa bado hai, Harani alikufa katika nchi alimozaliwa, katika jiji la Uru^e la Wakaldayo.^f **29** Abram na Nahori wakapata wake. Mke wa Abram aliitwa Sarai,^g na mke wa Nahori aliitwa Milka, binti ya Harani, baba ya Milka^h na Iska. **30** Sasa Sarai alikuwa tasa,ⁱ hakuwa na mtoto.

31 Kisha Tera akamchukua Abram mwanawe na Loti mjukuu wake,^j mwana wa Harani, na Sarai binti mkwe wake, mke wa Abram mwanawe, wakaondoka pamoja naye katika jiji la Uru la Wakaldayo ili kwenda katika nchi ya Kanaani.^k Baada ya muda wakafika Harani^l na kuanza kukaa huko. **32** Tera aliishi miaka 205. Kisha Tera akafa huko Harani.

12 Yehova akamwambia Abram: "Ondoka katika nchi yako na kutoka kwa watu wako wa ukoo na nyumba ya baba yako uende katika nchi nitakayokuonyesha;"^a **2** Nitakufanya kuwa taifa kubwa, nami nitakubariki, nami nitalifanya jina lako liwe kuu, nawe utakuwa baraka.^b **3** Nitawabariki wale wanaokubariki, nami nitawalaani wale wanaokulaani,^c na familia zote duniani hakika zitabarikiwa* kupitia kwako."^d

4 Basi Abram akaondoka kama Yehova alivyokuwa amemwambia, na Loti akaondoka pamoja naye. Abram alikuwa na umri wa miaka 75 alipoondoka Harani.^e **5** Abram akamchukua Sarai^f mke wake na Loti mwana wa ndugu yake^g na mali zote ambazo walikuwa wamekusanya^h na watu ambao walikuwa wamejipatia huko Harani, nao wakaanza safari ya kwenda katika nchi ya Kanaani.ⁱ Walipofika nchi ya Kanaani, **6** Abram akasafiri nchini mpaka eneo la Shekemu,^j karibu na miti mikubwa ya More.^k Wakati huo Wakanaani walikuwa katika nchi hiyo. **7** Kisha Yehova akamotokea Abram na kumwambia: "Nitaupa uzoa wako*^l nchi hii."^m Basi akamjengea Yehova madhabahu huko, aliyekuwa amemtokea. **8** Baadaye akatoka huko na kwenda katika eneo lenye milima upande wa mashariki wa Betheliⁿ na kupiga hema lake, jiji la Betheli likiwa upande wa magharibi na Ai^o upande wa mashariki. Huko, akamje-

12:3 *Au "zitajipatia baraka." 12:7 *Tnn., "Nitaipa mbegu yako."

SURA YA 12

- a Yos 24:3
Mdo 7:3, 4
- b Mwa 13:14, 16
Mwa 15:1, 5
Mwa 17:5
Mwa 22:17, 18
Kum 26:5
- c Mwa 27:29, 30
- d Mdo 3:25
Gal 3:8
- e Ebr 11:8
- f Mwa 11:29
- g Mwa 11:31
- h Mwa 13:5, 6
- i Mwa 26:3
- j Mdo 7:15, 16
- k Mwa 35:4
Kum 11:29, 30
- l Mwa 3:15
Mwa 21:12
Mwa 28:13, 14
Ro 9:7
Gal 3:16
- m Mwa 13:14, 15
Mwa 15:1, 7
Mwa 17:1, 8
Kum 34:4
- n Mwa 28:16-19
Mwa 31:13
- o Mwa 13:1, 3
Yos 7:2

Safu ya 2

- a Mwa 8:20
Mwa 35:2, 3
- b Mwa 26:25
- c Mwa 20:1
Mwa 24:62
- d Zb 105:13
- e Mwa 26:1, 2
- f Mwa 26:7
- g Mwa 20:11, 12
- h Mwa 20:14
Mwa 24:34, 35
- i Mwa 11:29
Mwa 17:15
Mwa 23:2, 19

negea Yehova^a madhabahu na kuanza kuliitia jina la Yehova.^b **9** Baadaye, Abram akavunja kambi na kusafiri kuelekea Negebu,^c akihamisha kambi yake kutoka sehemu moja hadi nyingine.

10 Sasa njaa kali ikatokea nchini, na Abram akatere-mka kuelekea Misri ili akae huko kwa muda fulani,^{*d} kwa sababu njaa hiyo ilikuwa kali sana.^e **11** Alipokaribia kuingia Misri, akamwambia Sarai mke wake: "Tafadhali sikiliza! Ninajua kwamba wewe ni mwanamke mrembo sana.^f

12 Kwa hiyo Wamisri watakapokuona, hakika watase-ma, 'Huyu ni mke wake.' Hala-fu wataniau, lakini wewe watakuacha hai. **13** Tafadhali waambie wewe ni dada yangu, ili mambo yaniendee vema kwa sababu yako, nao hawatania."^{*g}

14 Mara tu Abram alipoi-ngia Misri, Wamisri waliona kwamba mwanamke huyo alikuwa mrembo sana. **15** Na maofisa wa Farao walimwona pia, nao wakaanza kumsifu mbele ya Farao, kwa hiyo mwanamke huyo akapeleka katika nyumba ya Farao.

16 Farao alimtendea Abram vema kwa sababu ya Sarai, naye akapata kondoo, ng'o-mbe, punda madame na majike, watumishi wa kiume na wa kike, na ngamia.^h **17** Ndi-po Yehova akampiga Farao na watu wa nyumbani mwake kwa mapigo makali kwa sababu ya Sarai, mke wa Abram.ⁱ **18** Basi Farao akamwita Abram na kumuuliza:

12:10 *Au "aishi huko akiwa mgeni." 12:13 *Au "na nafsi yangu itaendelea kuishi."

“Kwa nini umenitendea hivi? Kwa nini hukuniambia kwa-mba yeye ni mke wako? **19** Kwa nini ulisema, ‘Huyu ni dada yangu,’^a hivi kwamba nilikuwa karibu kumchukua awe mke wangu? Mke wako ndiye huyu. Mchukue uende zako!” **20** Kwa hiyo Farao akawapa maafisa wake maagizo kumhusu, nao wakamwacha aende zake pamoja na mke wake na vyote alivyokuwa navyo.^b

13 Kisha Abramam akapanda kutoka Misri kwenda Negebu,^c yeye pamoja na mke wake na vitu vyote alivyokuwa navyo, pamoja na Loti. **2** Abramam alikuwa na utajiri mwingi wa mifugo, fedha, na dhahabu.^d **3** Alipiga kambi sehemu moja baada ya nyingine aliposafiri kutoka Negebu kwenda Betheli, mpaka alipofika mahali alipokuwa amepiga hema lake kati ya Betheli na Ai,^e **4** mahali alipokuwa amejenga madhabahu mwanzoni. Huko, Abramam akaliiitia jina la Yehova.

5 Sasa Loti, aliyekuwa akisafiri pamoja na Abramam, alikuwa pia na kondoo, ng’ombe, na mahema. **6** Basi wote hawangeweza kukaa pamoja kwa sababu nchi haikuwatoshia; mali zao zilikuwa zimeongezeka sana hivi kwamba hawangeweza tena kukaa pamoja. **7** Kwa sababu hiyo, ugomvi ukatokea kati ya wachungaji wa mifugo ya Abramam na wachungaji wa mifugo ya Loti. (Wakati huo Wakanaani na Waperizi walikuwa wakikaa katika nchi hiyo.)^f **8** Basi Abramam akamwambia Loti:^g “Tafadhali, pasiwe na ugomvi wowote

SURA YA 12

a Mwa 20:11, 12

b Zb 105:14

SURA YA 13

c Mwa 12:9

Mwa 20:1

d Mwa 24:34, 35

e Mwa 12:8, 9

Yos 7:2

f Mwa 10:19

g Mwa 11:27

Safu ya 2

a Mwa 19:28

b Mwa 2:8, 9

c Mwa 19:20-22

d Mwa 19:28, 29

e Mwa 18:20

Mwa 19:5

2Pe 2:6-8

Yud 7

f Mwa 12:7

Mwa 15:18

Mwa 24:7

Kut 33:1

kati yangu mimi na wewe na kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako, kwa maana sisi ni ndugu. **9** Je, nchi yote haiko mbele yako? Tafadhali, jitenge nami. Ukienda kushoto, nitakwenda kulia; lakini ukienda kulia, basi mimi nitakwenda kushoto.” **10** Kwa hiyo Loti akainua macho yake na kuona kwamba wilaya yote ya Yordani^a ilikuwa na maji ya kutosha (kabla Yehova hajaharibu Sodoma na Gomora), kama bustani ya Yehova,^b kama nchi ya Misri, mpaka Soari.^c **11** Basi Loti akajichagulia wilaya yote ya Yordani, naye Loti akahamisha kambi yake kuelekea upande wa mashariki. Kwa hiyo wakatengana. **12** Abramam aliishi katika nchi ya Kanaani, lakini Loti aliishi katika majiji ya wilaya hiyo.^d Hatimaye akapiga hema lake karibu na Sodoma. **13** Sasa watu wa Sodoma walikuwa waovu, nao walitenda dhambi nzito machoni pa Yehova.^e

14 Yehova akamwambia hivi Abramam baada ya Loti kujitenga naye: “Tafadhali, inua macho yako, na kutoka mahali ulipo tazama kaskazini na kusini, mashariki na magharibi, **15** kwa sababu nchi yote unayoona, nitakupa wewe na uzao wako* iwe miliki yenu ya kudumu.^f **16** Nami nitaufanya uzao wako uwe* kama chembe za mavumbi ya ardhi, hivi kwamba ikiwa kuna yeyote anayeweza kuhesabu chembe za mavumbi ya ardhi, basi uzao wako utaweza#

13:15 *Tnn., “mbegu yako.” 13:16

*Tnn., “nitaifanya mbegu yako iwe.”

#Tnn., “mbegu yako itaweza.”

kuhesabiwa.^a **17** Ondoka, safiri kwa mapana na marefu katika nchi hii, kwa maana nitakupa wewe nchi hii.”

18 Basi Abramam akaendelea kuishi katika mahema. Baada ya akaja na kuishi kati ya miti mikubwa ya Mamre,^b ambayo iko Hebroni,^c na huko akamjengea Yehova madhabahu.^d

14 Sasa katika siku za Amrafeli mfalme wa Shinari,^e Arioko mfalme wa Elasari, Kedorlaoma^f mfalme wa Elamu,^g na Tidali mfalme wa Goiimu, **2** wafalme hawa walikwenda kupigana vita na Bera mfalme wa Sodoma,^h Birsha mfalme wa Gomora,ⁱ Shinabu mfalme wa Adma, Shemeberi mfalme wa Seboiimu,^j na mfalme wa Bela, yaani, Soari. **3** Hao wote waliungana pamoja katika Bonde la* Sidimu,^k yaani, Bahari ya Chumvi.^l

4 Walikuwa wamemtumikia Kedorlaoma kwa miaka 12, lakini wakaasi katika mwaka wa 13. **5** Kwa hiyo katika mwaka wa 14, Kedorlaoma na wafalme waliokuwa pamoja naye wakaja na kuwashinda Warefaimu waliokuwa Ashteroth-karnaimu, Wazuzi waliokuwa Hamu, Waemi^m waliokuwa Shave-kiriathaimu, **6** na Wahoriⁿ katika mlima wao wa Seiri^o na kuteremka mpaka El-parani, eneo lililo nyikani. **7** Kisha wakarudi nyuma na kwenda Enmishpati, yaani, Kadeshi,^p wakashinda eneo lote la Waamaleki^q na pia Waamori^r waliokuwa wakiishi Hasason-tamari.^s

14:3, 8 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”

SURA YA 13

a Mwa 12:2
Mwa 15:1, 5
Kut 1:7
Ebr 11:12

b Mwa 18:1
Mwa 23:19
Mwa 25:9, 10
Mwa 35:27

c Mwa 23:2

d Mwa 12:7

SURA YA 14

e Mwa 10:9, 10

f Mwa 14:17

g Mwa 10:22

h Mwa 10:19
Mwa 13:12

i Mwa 13:10, 12

j Kum 29:23

k Mwa 14:10

l Hes 34:2, 12

m Kum 2:10, 11

n Kum 2:12

o Mwa 36:8

p Hes 20:1

q Mwa 36:12
1Sa 15:2

r Mwa 10:15, 16

s 2Nya 20:2

Safu ya 2

a Mwa 14:1, 2

b Mwa 14:16

c Mwa 19:1

d Mwa 13:18

e Mwa 14:24

f Mwa 11:27

g Amu 18:29

8 Ndipo mfalme wa Sodoma akapiga mwendo, na pia mfalme wa Gomora, mfalme wa Adma, mfalme wa Seboiimu, na mfalme wa Bela, yaani, Soari, nao wakajipanga kiwita ili kupigana nao katika Bonde la* Sidimu, **9** ili kupigana na Kedorlaoma mfalme wa Elamu, Tidali mfalme wa Goiimu, Amrafeli mfalme wa Shinari, na Arioko mfalme wa Elasari^a—wafalme wanne dhidi ya wale watano. **10** Sasa Bonde la Sidimu lilikuwa limejaa mashimo ya lami, na wafalme wa Sodoma na Gomora walijaribu kutoroka lakini wakaanguka humo, na wale waliobaki wakakimbilia eneo lenye milima. **11** Kisha washindi wakachukua mali zote za Sodoma na Gomora na chakula chao chote na kwenda zao.^b **12** Pia wakamchukua Loti, mwana wa ndugu ya Abramam ambaye alikuwa akikaa Sodoma,^c na vilevile wakachukua mali zake, wakaenda zao.

13 Baada ya hayo mtu mmoja aliyetoroka akaja na kumletea habari Abramam Mwebrania. Wakati huo alikuwa akiishi karibu na miti mikubwa ya Mamre yule Mwamori,^d ndugu ya Eshkoli na Aneri.^e Wanaume hao waliukuwa marafiki wa Abramam.

14 Hivyo Abramam akasikia kwamba mtu wake wa ukoo^{*f} alikuwa ametekwa. Kwa hiyo akawakusanya wanaume wake waliozoezwa, watumishi 318 waliozaliwa nyumbani mwake, wakawafuatia mpaka Dani.^g

15 Wakati wa usiku, akavigawa vikosi vyake, yeye na watumishi wake wakawashambulia

14:14 *Tnn., “ndugu yake.”

na kuwashinda. Naye akawafuatia mpaka Hoba, upande wa kaskazini wa Damasko. **16** Alipata mali zote zilizo-chukuliwa, na pia akamwokoa Loti mtu wake wa ukoo, mali zake, wanawake, na watu wengine.

17 Abramam aliporudi baada ya kumshinda Kedorlaoma na wafalme waliokuwa pamoja naye, mfalme wa Sodoma alienda kukutana na Abramam kwenye Bonde la* Shave, yaani, Bonde la Mfalme.^a **18** Na Melkizedeki^b mfalme wa Salemu^c akaleta mkate na divai; alikuwa kuhani wa Mungu Aliye Juu Zaidi.^d

19 Kisha akambariki Abramam na kumwambia:

“Abramam na abarikiwe na Mungu Aliye Juu Zaidi, Muumba wa mbingu na dunia;

20 Na asifiwe Mungu Aliye Juu Zaidi,

Ambaye amewatia mikononi mwako wale wanaokukandamiza!”

Na Abramam akampa sehemu ya kumi ya vitu vyote.^e

21 Baada ya hayo mfalme wa Sodoma akamwambia Abramam: “Nipe hao watu, lakini chukua mali.” **22** Lakini Abramam akamwambia mfalme wa Sodoma: “Ninauinua mkono wangu na kuapa kwa Yehova, Mungu Aliye Juu Zaidi, Muumba wa mbingu na dunia, **23** kwamba sitachukua kitu chochote ambacho ni chako, kuanzia uzi mpaka kamba ya kiatu, ili usije ukasema, ‘Nilitajirisha Abramam.’ **24** Sitachukua chochote isipokuwa

14:17 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”

SURA YA 14

a 2Sa 18:18

b Zb 110:4
Ebr 6:20

c Ebr 7:1, 2

d Zb 83:18
Ebr 5:5, 10

e Ebr 7:4

Safu ya 2

a Mwa 14:13

SURA YA 15

b Zb 27:1
Isa 41:10
Ro 8:31
Ebr 13:6c Kum 33:29
Met 30:5

d Mwa 17:5, 6

e Mwa 24:2, 3

f Mwa 12:7
Mdo 7:5g Mwa 17:15, 16
Mwa 21:12h Mwa 22:17
Kum 1:10
Ro 4:18
Ebr 11:12

i Ebr 11:8

j Ro 4:13, 22
Gal 3:6
Yak 2:23k Mwa 11:31
Ne 9:7

kile ambacho wanaume hawa vijana wamekula tayari. Lakini kuhusu fungu la watu walioenda pamoja nami, Aneri, Eshkoli, na Mamre^a—acha wachukue fungu lao.”

15 Baada ya hayo neno la Yehova likamjia Abramam katika maono, likisema: “Usiogope,^b Abramam. Mimi ni ngao yako.^c Thawabu yako itakuwa kubwa sana.”^d **2** Abramam akasema: “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, utanipani nini, kwa sababu mpaka sasa sina mtoto na yule atakayerithi nyumba yangu ni Eliezeri,^e mtu wa Damasko?” **3** Abramam akaendelea kusema: “Hujanipa uzao wowote,^f na mtu^g wa nyumba yangu atakuwa mrithi wangu.” **4** Lakini tazama! Yehova akamjibu hivi: “Mtu huyu hatakuwa mrithi wako, lakini mwana wako mwenyewe^{*} atakuwa mrithi wako.”^g

5 Ndipo akamtoa nje na kumwambia: “Tafadhali, tazama juu mbinguni uzihesabu nyota, ikiwa unaweza kuzihesabu.” Kisha akamwambia: “Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.”^h **6** Naye akawa na imani katika Yehova,ⁱ Naye akamhesabu kuwa mwadilifu.^j **7** Pia akasema hivi: “Mimi ni Yehova, niliyekutoa katika jiji la Uru la Wakaldayo ili nikupe nchi hii iwe miliki yako.”^k **8** Ndipo Abramam akauliza: “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, nitajuaje kwamba nitaimiliki?”

15:3 *Tnn., “mbegu yoyote.” ^gTnn., “mwana.” 15:4 *Tnn., “yule anayetoka katika sehemu zako za ndani.” 15:5 *Tnn., “itakavyokuwa mbegu yako.” 15:6 *Au “akamhesabia uadilifu.”

9 Mungu akamjibu: “Chukua kwa ajili yangu ndama jike wa miaka mitatu, mbuzi jike wa miaka mitatu, kondoo dume wa miaka mitatu, njiwa tetere, na njiwa mchanga.” **10** Basi akawachukua wote hao na kuwakata vipande viwili na kuweka kila kipande kando ya kipande cha pili,* lakini hakuwakata ndege. **11** Kisha ndege wawindaji wakaanza kushuka juu ya mizoga hiyo, lakini Abram u akawa akiwafukuza.

12 Jua lilipokaribia kutua, usingizi mzito ukamshika Abram u na giza zito lenye kuogopesha likamfunika. **13** Kisha Mungu akamwambia Abram u: “Ujue kwa hakika kwamba wazao* wako watakuwa wageni katika nchi ambayo si yao na kwamba watu wa nchi hiyo watawafanya kuwa watumwa na kuwatesa kwa miaka 400.^a **14** Lakini mimi nitalihukumu taifa watakalolitumikia,^b na baada ya hapo watatoka huko na mali nyingi.^c **15** Lakini wewe, utaenda kwa mababu zako kwa amani; utazikwa baada ya kuishi maisha marefu.^d **16** Lakini wazao wako watarudi hapa^e katika kizazi cha nne, kwa sababu uovu wa Waamori bado haujifikia kipimo chake kamili.”^f

17 Jua lilipotua na giza zito kuingia, tanuru linalofuka moshi lilitokea, na mwenge wa moto ukapita katikati ya vile vipande vya nyama. **18** Siku hiyo Yehova alifanya agano^g pamoja na Abra-

15:10 *Au “na kuweka kila kipande ili kilingane na cha pili.” 15:13 *Tnn., “mbegu.”

SURA YA 15

a Mwa 21:9
Kut 1:13, 14
Kut 3:7
Mdo 7:6, 7

b Kut 7:4
Hes 33:4

c Kut 3:22
Zb 105:37

d Mwa 25:8

e Yos 14:1
Mdo 7:7

f 1Fa 21:26
2Fa 21:11

g Mwa 17:19
Mwa 22:17

Safu ya 2

a Kut 3:8

b 1Fa 4:21

c 1Sa 15:6

d Yos 1:4

e Kut 3:17

f Yos 17:15

g Kum 7:1

SURA YA 16

h Mwa 15:2, 3

i Gal 4:25

j Mwa 30:1, 3

mu, akisema: “Nitaupa uzao wako* nchi hii,^a kuanzia mto wa Misri mpaka kwenye ule mto mkubwa, mto Efrati:^b **19** nchi ya Wakeni,^c Wakenizi, Wakadmoni, **20** Wahiti,^d Waperizi,^e Warefaimu,^f **21** Waamori, Wakanaani, Wagirgashi, na Wayebusi.”^g

16 Sasa Sarai mke wa Abram u hakuwa amezalia mtoto yeyote,^h lakini alikuwa na mtumishi Mmisri aliyeitwa Hagari.ⁱ **2** Basi Sarai akamwambia Abram u: “Sasa tafadhali! Yehova amenizuia nisizae watoto. Tafadhali, lala na mtumishi wangu. Huenda nikapata watoto kupitia yeye.”^j Kwa hiyo Abram u akasikiliza maneno ya Sarai. **3** Baada ya Abram u kuishi katika nchi ya Kanaani kwa miaka kumi, Sarai mke wa Abram u akamchukua Hagari, mtumishi wake Mmisri na kumpa Abram u mumewe awe mke wake. **4** Basi Abram u akalala na Hagari, naye akapata mimba. Alipogundua kwamba ana mimba, alianza kumdharau bimbubwa wake.

5 Ndipo Sarai akamwambia Abram u: “Ni wewe uliyesababisha madhara ninayotendewa. Ni mimi niliyemweka mtumishi wangu mikononi mwako,* lakini alipogundua kwamba ana mimba, alianza kunidharau. Yehova na awe mwamuzi kati yangu na wewe.” **6** Basi Abram u akamwambia Sarai: “Tazama! Mtumishi wako yuko chini ya mamlaka yako. Mtendee lolote unaloona ni jema.” Kisha

15:18 *Tnn., “Nitaipa mbegu yako.” 16:5 *Tnn., “kifuani pako.”

Sarai akamfedhehesha Hagari, naye akamkimbia.

7 Baadaye malaika wa Yehova akamkuta kwenye chemchemi ya maji nyikani, chemchemi iliyo njiani kuelekea Shuri.^a **8** Naye akamuuliza: “Hagari, mtumishi wa Sarai, umetoka wapi na unaenda wapi?” Ndipo akajibu: “Ninamkimbia Sarai, bimbubwa wangu.” **9** Basi malaika wa Yehova akamwambia: “Rudi kwa bimbubwa wako na ujinyenyekeze chini ya mkono wake.” **10** Kisha malaika wa Yehova akasema: “Nitawazidisha sana wazao wako, hivi kwamba watakuwa wengi sana wasiweze kuhesabiwa.”^b **11** Malaika wa Yehova akaendelea kusema: “Sasa una mimba, nawe utazaa mwana, nawe unapaswa kumpa jina Ishmaeli,* kwa maana Yehova amesikia mateso yako. **12** Atakuwa mtu aliye kama pundamwitu.* Mkono wake utapigana na kila mtu, na mkono wa kila mtu utapigana naye, naye atakaa akielekeana na ndugu zake wote.”[#]

13 Ndipo akaliitia jina la Yehova, aliyekuwa akizungumza naye: “Wewe ni Mungu anayeona,”^c kwa kuwa alisema: “Je, ni kweli kwamba nime mwona hapa yeye ambaye huniona?” **14** Ndiyo sababu kisima hicho kiliitwa Beer-lahai-roi.* (Kiko kati ya Kadeshi na Beredi.) **15** Basi Hagari akamzalia Abramumwana, naye

16:11 *Maana yake “Mungu Husikia.” **16:12** *Baadhi ya watu hudhani ni pundamilia. Yaelekea ametumiwa kurejelea mtazamo wa kujitegemea. [#] Au labda, “naye ataishi kwa uhasama na ndugu zake wote.” **16:14** *Maana yake “Kisima cha Aliye Hai Ambaye Huniona.”

SURA YA 16

a Mwa 25:17, 18
Kut 15:22

b Mwa 17:20
Mwa 25:13-16
1Nya 1:29-31

c Met 15:3

Safu ya 2

a Mwa 21:9
Gal 4:22, 24

SURA YA 17

b Mwa 15:18
Zb 105:8-11

c Mwa 22:17
Kum 1:10
Ebr 11:11, 12

d Zb 105:9-11

e Mwa 13:16
Ro 4:17

f Mwa 35:10, 11

g Lu 1:72, 73

h Kut 6:4
Ebr 11:8, 9

i Kum 14:2

Abramu akamwita huyo mwana ambaye Hagari alimzaa, Ishmaeli.^a **16** Abramum alikuwa na umri wa miaka 86 Hagari alipomzaa Ishmaeli.

17 Abramum alipokuwa na umri wa miaka 99, Yehova alimtokea na kumwambia: “Mimi ni Mungu Mweza-Yote. Tembea mbele zangu na ujithibitisha mwenyewe kuwa bila kosa.* **2** Nitaimarisha agano langu kati yangu na wewe,^b nami nitawafanya wazao wako wawe wengi, wengi sana.”^c

3 Ndipo Abramum akaanguka kifudufudi, na Mungu akaendelea kuongea naye, na kumwambia: **4** “Mimi nami, tazama! agano langu liko pamoja nawe,^d nawe hakika utakuwa baba wa mataifa mengi.^e **5** Jina lako halitakuwa tena Abramum;* jina lako litakuwa Abrahamum,^f kwa sababu nitakufanya kuwa baba wa mataifa mengi. **6** Nitakufanya uwe na wazao wengi, wengi sana, nami nitakufanya uwe mataifa, na wafalme watatoka kwako.^f

7 “Nami nitalishika agano langu nililofanya pamoja nawe^g na uzao wako* baada yako katika vizazi vyao vyote; hili ni agano la milele, ili niwe Mungu wako na Mungu wa uzao wako* baada yako. **8** Nami nitakupa wewe na uzao wako* baada yako nchi ambamo uliishi ukiwa mgeni^h—nchi yote ya Kanaani—iwe miliki ya kudumu, nami nitakuwa Mungu wao.”ⁱ

17:1 *Au “bila lawama.” **17:5** *Maana yake “Baba Yuko Juu (Amekwezwa).” [#]Maana yake “Baba wa Umati (Halaiki); Baba wa Wengi.” **17:7, 8** *Tnn., “mbe-gu yako.”

9 Mungu akaendelea kumwambia Abrahamu: “Wewe nawe, unapaswa kushika agano langu, wewe na uzao wako* baada yako katika vizaizi vyao vyote. **10** Hili ndilo agano langu nililofanya pamoja nawe, ambalo wewe na uzao wako* baada yako mtalishika: Kila mwanamume miongoni mwenu ni lazima atahiriwe.^a **11** Ni lazima mtahiri nyama ya magovi yenu, na jambo hilo litakuwa ishara ya agano kati yangu nanyi.^b **12** Katika vizaizi vyenu vyote, kila mwanamume miongoni mwenu mwenye umri wa siku nane ni lazima atahiriwe,^c yeyote anayezaliwa nyumbani mwenu na yeyote ambaye si mmoja wa uzao wenu* na yeyote aliyenunuliwa kwa pesa kutoka kwa mgeni. **13** Kila mwanamume aliyezaliwa nyumbani mwenu na kila mwanamume aliyenunuliwa kwa pesa zenu ni lazima atahiriwe,^d na agano langu katika miili yenu litakuwa agano la kudumu. **14** Ikiwa mwanamume yeyote ambaye hajatahiriwa hatatahiri nyama ya govi lake, ni lazima auawe. Amevunja agano langu.”

15 Kisha Mungu akamwambia Abrahamu: “Kuhusu mke wako Sarai,^e usimwite tena Sarai, kwa sababu jina lake litakuwa Sara.[#] **16** Nitambariki na pia nitakupua mwana kupitia yeye;^f nitambariki Sara, naye atakuwa mataifa; wafalme wa mataifa watatoka kwake.” **17** Ndi-po Abrahamu akaanguka ki-

17:9, 10 *Tnn., “mbegu yako.” 17:12 *Tnn., “mbegu yenu.” 17:15 *Huenda jina hili linamaanisha “Mgomvi.” #Maana yake “Binti ya Mfalme.”

SURA YA 17

a Mwa 21:4
Ro 2:29

b Mdo 7:8
Ro 4:11

c Lu 2:21

d Kut 12:44

e Mwa 11:29

f Mwa 18:10

Safu ya 2

a Mwa 18:12

b Ro 4:19
Ebr 11:11

c Mwa 16:11

d Mt 1:2

e Mwa 26:24

f Mwa 16:10
Mwa 21:13, 18
Mwa 25:13-16
1Nya 1:29-31

g Mwa 26:3
Ebr 11:8, 9

h Mwa 18:10, 14
Mwa 21:1

i Mwa 17:13

j Mdo 7:8
Ro 4:11

fudufudi, akaanza kucheka na kusema moyoni mwake:^a “Je, mwanamume mwenye umri wa miaka 100 atazaa mtoto, na je, Sara, mwanamke mwenye umri wa miaka 90, atazaa?”^b

18 Kwa hiyo Abrahamu akamwambia Mungu wa kweli: “Afadhali umbariki Ishmaeli ili aendelee kuishi!”^c **19** Ndi-po Mungu akasema: “Mke wako Sara hakika atakuzalia mwana, nawe unapaswa kumpa jina Isaka.^d Nami nitamarisha agano langu pamoja naye liwe agano la milele kwa uzao wake[#] baada yake.^e **20** Lakini kuhusu Ishmaeli, nimesikia ombi lako. Tazama! Nitambariki, nami nitamfanya awe na wazao wengi, nao wataongezeka na kuwa wengi, wengi sana. Atazaa wakuu 12, nami nitamfanya awe taifa kubwa.^f **21** Hata hivyo, nitamarisha agano langu pamoja na Isaka,^g ambaye Sara atakuzalia wakati huuhuu mwaka ujao.”^h

22 Mungu alipomaliza kuzungumza na Abrahamu, alipanda na kumwacha Abrahamu. **23** Kisha Abrahamu akamchukua Ishmaeli mwana wake na wanaume wote waliozaliwa nyumbani mwake na kila mwanamume aliyekuwa amemnunua kwa pesa, kila mwanamume katika nyumba ya Abrahamu, naye akawatahiri nyama ya magovi yao siku hiyohiyo, kama Mungu alivyokuwa amemwambia.ⁱ **24** Abrahamu alikuwa na umri wa miaka 99 alipotahiriwa nyama ya govi lake.^j **25** Na Ishmaeli mwanawe alikuwa na umri wa mia-

17:19 *Maana yake “Kicheko.” #Tnn., “mbegu yake.”

ka 13 alipotahiriwa nyama ya govi lake.^a **26** Siku hiyohiyo, Abrahamu alitahiriwa na pia Ishmaeli mwanawe. **27** Wanaume wote wa nyumba yake, yeyote aliyezaliwa nyumbani mwake na yeyote aliyenunuliwa kwa pesa kutoka kwa mgeni, walitahiriwa pia pamoja naye.

18 Baadaye, Yehova^{*b} akamotokea kati ya miti mikubwa ya Mamre^c alipokuwa ameketi kwenye mlango wa hema mchana wakati wa joto kali. **2** Akainua macho yake na kuwaona wanaume watatu wakiwa wamesimama umbali fulani kutoka kwake.^d Alipowaona, alikimbia kutoka kwenye mlango wa hema na kwenenda kuwapokea, naye akainama mpaka chini. **3** Kisha akasema: "Yehova, ikiwa nimepata kibali machoni pako, tafadhali usinipite mimi mtumishi wako. **4** Tafadhali, acheni maji kidogo yaletwe ili mwoshwe miguu yenu;^e kisha mpumzike chini ya mti. **5** Kwa sababu mmekuja hapa kwangu mimi mtumishi wenu, acheni nilete kipande cha mkate ili mjiburudishe.* Kisha mnaweza kuendelea na safari yenu." Ndipo wakasema: "Ni sawa. Unaweza kufanya kama ulivyosema."

6 Kwa hiyo Abrahamu akainda haraka hemani na kumwambia Sara: "Fanya haraka! Chukua vipimo vitatu* vya unga laini, ukande unga huo, na kuoka mikate." **7** Kisha

18:1 *Yaani, malaika aliyemwakilisha Yehova. **18:5** *Tnn., "mtie nguvu mioyo yenu." **18:6** *Tnn., "vipimo vitatu vya sea." Sea moja ilikuwa sawa na lita 7.33 (vibaba 6.66). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 17
a Mwa 16:16

SURA YA 18
b Mwa 16:7
Amu 13:21

c Mwa 13:18
Mwa 14:13

d Mwa 19:1

e Mwa 19:2
Mwa 24:32

Safu ya 2

a Ebr 13:2

b Mwa 17:15

c Mwa 17:21
Mwa 21:2
Ro 9:9

d Mwa 17:17

e Ro 4:19

f Ebr 11:11
1Pe 3:6

g Isa 40:29
Mt 19:26
Lu 1:36, 37

Abrahamu akakimbia kwenenda kwenye mifugo, akachagua ng'ombe dume mchanga, mzuri na laini. Akampa mtumishi wake, naye akafanya haraka kumtayarisha. **8** Halafu akachukua siagi na maziwa na huyo ng'ombe dume mchanga ambaye alikuwa amemtayarisha, akaviweka vyakula hivyo mbele yao. Kisha akasimama kando yao chini ya mti walipokuwa wakila.^a

9 Wakamuuliza: "Yuko wapi Sara mke wako?"^b Akajibu: "Yumo humu hemani."

10 Kwa hiyo mmoja wao akasema: "Kwa hakika nitarudi kwako mwaka ujao wakati huuhuu, na tazama! mke wako Sara atakuwa na mwana."^c Sasa Sara alikuwa akisikiliza kwenye mlango wa hema uliokuwa nyuma ya mtu huyo.

11 Abrahamu na Sara ulikuwa wazee, umri wao ulikuwa umesonga.^d Sara alikuwa amepita umri wa kuzaa watoto.^e

12 Kwa hiyo Sara akainza kucheka kimoyomoyo na kusema: "Nikiwa mkongwe hivi na bwana wangu akiwa amezeeka, ninaweza kweli kupata shangwe hii?"^f

13 Kisha Yehova akamwambia Abrahamu: "Kwa nini Sara amecheka na kusema, 'Je, kweli nitazaa mtoto nikiwa nimezeeka?'"

14 Je, kuna jambo lolote lisi lowezekana kwa Yehova?^g Nitarudi kwako mwaka ujao wakati huuhuu, na Sara atakuwa na mwana." **15** Lakini Sara akakana akisema, "Mimi siku cheka!" kwa maana aliogopa. Ndipo Mungu akamwambia: "Hakika! Ulicheka."

18:11 *Yaani, "Alikuwa ameacha kupata hedhi."

16 Wanaume hao waliposimama ili kuondoka Abrahamu aliwasindikiza, waka-tazama chini kuelekea Sodoma.^a **17** Yehova akasema: "Kwa nini nimfiche Abrahamu jambo ninalokusudia kufanya?"^b **18** Kwa hakika Abrahamu atakuwa taifa kubwa na lenye nguvu, na mataifa yote ya dunia yatabarikiwa* kupitia yeye.^c **19** Kwa maana sasa nimemjua ili awaamuru watoto wake na nyumba yake baada yake kushika njia ya Yehova kwa kutenda yaliyo sawa na ya haki,^d ili Yehova atimize mambo aliyohidi kumhusu Abrahamu."

20 Kisha Yehova akasema: "Kilio dhidi ya Sodoma na Gomora kwa kweli ni kikubwa,^e na dhambi yao ni nzito sana.^f **21** Nitashuka chini ili nione kama mambo wanayotenda yanalingana na kilio kilichonifikia. Na kama sivyo, nitajua."^g

22 Kisha wanaume hao wakatoka huko na kuelekea Sodoma, lakini Yehova^h akabaki na Abrahamu. **23** Kisha Abrahamu akamkaribia na kumuuliza: "Je, kweli utamfagilia mbali mwadilifu pamoja na mwovu?"ⁱ **24** Tuseme kuna watu 50 waadilifu katika jiji hilo. Je, kweli utawafagilia mbali na hutalisamehe jiji hilo kwa ajili ya waadilifu hao 50 waliomo? **25** Ni jambo usiloweza kuwazia kumuua mwadilifu pamoja na mwovu hivi kwamba mtu mwadilifu apatwe na jambo lililele lilalompata mwovu!^j Ni jambo usiloweza kuwazia.^k Je, Mwamuzi wa dunia yote hatatenda jambo la haki?"^l **26** Ki-

18:18 *Au "yatajipatia baraka."

SURA YA 18

a Mwa 13:12

b Zb 25:14
Amo 3:7

c Mwa 12:1-3
Gal 3:14

d Kum 4:9

e 2Pe 2:7, 8

f Mwa 13:13
Yud 7

g Mwa 11:5
Kut 3:7, 8
Zb 14:2

h Mwa 31:11
Mwa 32:30

i Hes 16:22

j Zb 37:10, 11
Met 29:16
Mal 3:18
Mt 13:49

k Kum 32:4

l Ayu 34:12
Isa 33:22

Safu ya 2

a Hes 14:18
Zb 86:15

b Kut 34:6

c Mwa 18:2, 22

SURA YA 19

d Mwa 18:2, 22

sha Yehova akasema: "Nikipata watu 50 waadilifu katika jiji la Sodoma, nitalisamehe jiji lote kwa ajili yao." **27** Lakini Abrahamu akasema tena: "Tafadhali, nimethubutu kuzungumza nawe, Yehova, ijapokuwa mimi ni mavumbi na majivu. **28** Tuseme waadilifu hao 50 wapungue watano. Je, utaliangamiza jiji lote kwa sababu ya hao watano?" Akajibu: "Sitaliangamiza nikipata waadilifu 45 humo."^a

29 Lakini kwa mara nyingine tena akamwambia: "Tuseme 40 wapatikane humo." Akamjibu: "Sitaliangamiza kwa ajili ya hao 40." **30** Lakini akaendelea kusema: "Tafadhali Yehova, usiwake hasira,^b niruhusu niendeleo kuongea: Tuseme ni 30 tu wanaopatikana humo." Akamjibu: "Sitaliangamiza nikipata 30 humo." **31** Lakini akaendelea kusema: "Tafadhali, nimethubutu kuzungumza nawe, Yehova: Tuseme ni 20 tu wanaopatikana humo." Mungu akamjibu: "Sitaliangamiza kwa ajili ya hao 20." **32** Mwishowe akasema: "Tafadhali Yehova, usiwake hasira, lakini niruhusu niongee kwa mara ya mwisho: Tuseme ni kumi tu wanaopatikana humo." Akamjibu: "Sitaliangamiza kwa ajili ya hao kumi." **33** Yehova alipomaliza kuzungumza na Abrahamu, alienda zake^c na Abrahamu akarudi nyumbani kwake.

19 Wale malaika wawili wakafika Sodoma jioni, na Loti alikuwa ameketi katika lango la Sodoma. Loti alipo-waona, akasimama ili awapokee, akainama chini kifudufu-di.^d **2** Naye akasema: "Tafadhali, bwana zangu, tafadhali,

karibuni nyumbani mwangu mimi mtumishi wenu, mlale hapa usiku wa leo, nasi tuioshe miguu yenu. Kisha mna-weza kuamka asubuhi na mapema na kuendelea na safari yenu.” Wakamwambia: “Hapana, tutakaa usiku kucha kwenye uwanja wa jiji.” **3** Lakini akawasihi sana hivi kwamba wakaingia pamoja naye ndani ya nyumba yake. Kisha akawaandalia karamu, akaoka mikate isiyo na chachu, nao wakala.

4 Kabla hawajalala, wanaume wa jiji—wanaume wa Sodomu kuanzia mvulana mpaka mzee, wote—wakaizingira nyumba hiyo wakiwa umati. **5** Nao walikuwa wakimwambia Loti kwa sauti: “Wako wapi wale wanaume waliokuja kwako usiku wa leo? Walete nje kwetu ili tufanye nao ngono.”^a

6 Ndipo Loti akatoka nje kukutana nao mlangoni, naye akaufunga mlango nyuma yake. **7** Akasema: “Tafadhali, ndugu zangu, msitende uovu. **8** Tafadhali, humu nina mabinti wawili ambao hawajawahi kufanya ngono na mwanamume. Tafadhali, acheni niwalete nje kwenu muwatendee lolote mnaloo-na kuwa jema. Lakini msiwatendee lolote wanaume hawa, kwa sababu wamekuja chini ya kivuli cha* paa langu.”^b

9 Ndipo wakasema: “Ondoka!” Halafu wakasema: “Mgeni huyu aliye peke yake alikuja kuishi hapa, na sasa anathubutu kutuhukumu! Sasa tutakutendea wewe jambo baya zaidi kuliko wao.” Wakamzi-

19:8 *Au “ulinzi wa.”

SURA YA 19

a Yud 7

b Amu 19:23, 24

Safu ya 2

a Mwa 13:13
Mwa 18:20

b Lu 17:28

ngira Loti na kumbana* na kusogea mbele ili wauvunje mlango. **10** Basi wale wanaume* wakanyoosha nje mikonu yao na kumwingiza Loti ndani ya nyumba waliomokuwa, nao wakafunga mlango. **11** Lakini wakawapiga kwa upofu wanaume waliokwa mlangoni, kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi, hivi kwamba wakajichosha wakijaribu kuutafuta mlango.

12 Kisha wale wanaume* wakamwambia Loti: “Je, una mtu mwingine yeyote hapa? Wakwe zako, wanao, mabinti wako, na watu wengine wote wa ukoo jijini, waondoe mahali hapa! **13** Kwa maana tuliangamiza jiji hili, kwa sababu kilio dhidi ya wakaa-ji wake kwa kweli kimeongezeka sana* mbele za Yehova,^a hivi kwamba Yehova ametutuma tuliangamize jiji hili.” **14** Kwa hiyo Loti akatoka nje na kuanza kuzungumza na wakwe zake ambao wangewaoa mabinti zake, akawaambia tena na tena: “Ondokeni! Ondokeni mahali hapa, kwa sababu Yehova ataliangamiza jiji hili!” Lakini machoni pa wakwe zake alionekana kama mtu anayefanya mzaha.^b

15 Kulipokuwa kukipambazuka, malaika wakaanza kumhimiza Loti kwa uharaka, wakisema: “Fanya haraka! Mchukue mke wako na mabinti wako wawili walio hapa pamoja nawe, ili usifagiliwe mbali pamoja na uovu wa jiji hili!”^c **16** Alipozidi kukawia, basi kwa sababu Yehova

19:9 *Au “Wakasongamana kumzunguka Loti.” 19:10, 12 *Yaani, malaika waliovaa miili ya kibinadamu. 19:13 *Au “kimekuwa kikubwa.”

c Lu 17:29-31

alimhurumia,^a wale wanau-me* wakaushika mkono wake na mkono wa mke wake na mkono ya mabinti zake wawili, wakamtoa na kumpeleka nje ya jiji.^b **17** Mara tu walipokuwa wamewatoa nje ya jiji, mmoja wao akawaambia: “Kimbieni msije mkafa! Msitazame nyuma^c wala msisimame mahali popote katika wilaya hii!^d Kimbilieni eneo lenye milima msije mkafagiliwa mbali!”

18 Kisha Loti akawaambia: “Tafadhali Yehova,* acha ni-siende huko! **19** Sasa tafadhali, mimi mtumishi wako nimepata kibali machoni pako, nawe unanionyesha fadhili nyingi* kwa kunihifadhi hai,^e lakini siwezi kukimbilia eneo lenye milima kwa sababu ninaogopa kwamba huenda msiba ukanikumba nami nikafa.^f **20** Sasa tafadhali, mji huu uko karibu nami ninaweza kukimbilia humo; ni mji mdogo tu. Tafadhali, ninaweza kukimbilia humo? Ni mji mdogo tu. Kisha nitaokoka.”* **21** Kwa hiyo akamwambia: “Sawasawa, nitakutendea pia kwa fadhili,^g sitauangamiza mji uliotaja.^h **22** Fanya haraka! Kimbilia huko, kwa sababu sitafanya jambo lolote mpaka utakapofika huko!”ⁱ Ndiyo sababu aliuita mji huo Soari.*^j

23 Jua lilikuwa limechomozia nchini Loti alipofika Soari. **24** Kisha Yehova akaleta mvua ya kiberiti na moto juu ya Sodoma na Gomora—ilito-

19:16 *Yaani, malaika waliovaa miili ya kibinadamu. **19:18** *Yaani, malaika waliomwakilisha Yehova. **19:19** *Au “upendo mshikamanifu.” **19:20** *Au “nafsi yangu itaendelea kuishi.” **19:22** *Maana yake “Udogo.”

SURA YA 19

a Kut 33:19

b 2Pe 2:7-9

c Lu 9:62

d Mwa 13:10

e Zb 143:11

f Zb 6:4

g Zb 34:15

h Mwa 19:30
Zb 68:20

i 2Pe 3:9

j Mwa 14:2

Safu ya 2

a Kum 29:23
Lu 17:29
2Pe 2:6

b Mwa 13:10

c Lu 17:32
Ebr 10:38

d Mwa 18:2, 22

e Yud 7

f 2Pe 2:7, 8

g Mwa 19:17

h Mwa 19:20, 22

ka kwa Yehova, kutoka mbinguni.^a **25** Kwa hiyo akayaangamiza majiji hayo, naam, wilaya yote, pamoja na wakaaji wote wa majiji hayo na mimea yote.^b **26** Lakini mke wa Loti, aliyekuwa nyuma ya Loti, akaanza kutazama nyuma, naye akawa nguzo ya chumvi.^c

27 Sasa Abrahamu akaamka asubuhi na mapema na kwenda mahali alipokuwa amesimama mbele za Yehova.^d **28** Alipotazama chini kuelekea Sodoma na Gomora na nchi yote ya wilaya hiyo, aliona jambo la kushangaza. Kulikuwa na moshi mzito uliokuwa ukipanda juu kutoka nchini kama moshi mzito wa tanuru!^e **29** Kwa hiyo Mungu alipoyaangamiza majiji ya wilaya hiyo, Mungu alimkumbuka Abrahamu kwa kumtoa Loti katika majiji aliyoyaangamiza, ambamo Loti alikuwa akiishi.^f

30 Baadaye Loti akapanda kutoka Soari pamoja na mabinti zake wawili na kuanza kuishi katika eneo lenye milima,^g kwa sababu aliogopa kuishi Soari.^h Kwa hiyo akaanza kuishi pangoni pamoja na mabinti zake wawili. **31** Na mzaliwa wa kwanza akamwambia mdogo: “Baba yetu amezeeka, na hakuna mwanamume yeyote nchini anayeweza kulala nasi kama ilivyo desturi ya dunia yote. **32** Basi, tumpe baba yetu divai anywe, kisha tulale naye na kuhifadhi uzao wa baba yetu.”

33 Basi usiku huo wakampa baba yao divai nyingi anywe; kisha mzaliwa wa kwanza

19:28 *Au “kalibu.”

akaingia ndani na kulala na baba yake, lakini baba yake hakujua wakati alipolala naye wala alipoondoka. **34** Kisha siku iliyofuata, mzaliwa huyo wa kwanza akamwambia mdogo: "Jana usiku nililala na baba yetu. Na tumpe divai anywe usiku wa leo pia. Kisha uingie ndani na kulala naye, ili tuhifadhi uzao wa baba yetu." **35** Basi usiku huo pia wakampa baba yao divai nyingi anywe; kisha yule binti mdogo akaingia ndani na kulala naye, lakini baba yake hakujua wakati alipolala naye wala alipoondoka. **36** Kwa hiyo mabinti wote wawili wa Loti wakapata mimba kutoka kwa baba yao. **37** Mzaliwa wa kwanza alizaa mwana na kumpa jina Moabu.^a Yeye ndiye baba ya Wamoabu wa leo.^b **38** Yule mdogo pia alizaa mwana, akampa jina Benami. Yeye ndiye baba ya Waamoni^c wa leo.

20 Sasa Abrahamu akaihamisha kambi yake kutoka huko^d na kwenda katika nchi ya Negebu, akaanza kuishi kati ya Kadeshi^e na Shuri.^f Alipokuwa akiishi* Gerari,^g **2** Abrahamu akasema tena kumhusu Sara mke wake: "Huyu ni dada yangu."^h Kwa hiyo Abimeleki mfalme wa Gerari akaagiza Sara aletwe, naye akamchukua.ⁱ **3** Baada-ye, Mungu akamjia Abimeleki katika ndoto usiku na kumwambia: "Wewe ni kama mtu aliyekufa kwa sababu ya mwanamke huyu uliyemchukua,^j kwa maana ameolewa naye ni mke wa mwanamume mwingine."^k **4** Hata hivyo, Abimeleki ha-

20:1 *Au "akiishi akiwa mgeni."

SURA YA 19

a Kum 2:9

b 1Nya 18:2

c Kum 2:19
Amu 11:4
Ne 13:1
Sef 2:9

SURA YA 20

d Mwa 13:18

e Hes 13:26

f Mwa 25:17, 18

g Mwa 10:19
Mwa 26:6h Mwa 12:11-13
Mwa 20:11, 12

i Mwa 12:15

j Mwa 12:17
Zb 105:14

k Kum 22:22

Safu ya 2
a Zb 105:14, 15

b Ayu 42:8

c Mwa 12:18, 19
Mwa 26:9, 10d Mwa 12:11, 12
Mwa 26:7

kuwa amemkaribia.* Kwa hiyo akasema: "Yehova, je, utaliua taifa ambalo kwa kweli halina hatia?"^a **5** Je, yeye hakunia-mbia, 'Huyu ni dada yangu,' na mwanamke huyu pia hakunia-mbia, 'Huyu ni ndugu yangu?' Nilifanya jambo hili kwa moyo mnyoofu na mikono isiyona hatia." **6** Kisha Mungu wa kweli akamwambia katika ndoto: "Ninajua kwamba ulifanya jambo hili kwa moyo mnyoofu, kwa hiyo nilikuzuia usinitendee dhambi. Ndiyo sababu sikukuruhusu umguse. **7** Sasa mrudishe mke wa mwanamume huyo, kwa maana mwanamume huyo ni nabii,^a atakuombea dua,^b nawe utaendelea kuishi. Lakini usipomrudisha, ujue kwamba kwa hakika utakufa, wewe na watu wako wote."

8 Abimeleki akaamka asubuhi na mapema akawaita watumishi wake wote na kuwambia mambo hayo yote, nao wakaogopa sana. **9** Kisha Abimeleki akamwita Abrahamu na kumwambia: "Ni jambo gani hili ulilotutendea? Nimekutendea dhambi gani hivi kwamba umeniletea mimi na ufalme wangu dhambi kubwa hivi? Jambo ulilonitendea si sawa." **10** Na Abimeleki akaendelea kumwambia Abrahamu: "Ulikuwa na nia gani ulipofanya jambo hili?"^c **11** Abrahamu akasema: "Ni kwa sababu nilisema moyoni mwangu, 'Hakika watu wa mahali hapa hawamwogopi Mungu, nao watanuia kwa sababu ya mke wangu.'^d **12** Na isitoshe, kwa

20:4 *Yaani, hakuwa amefanya naye ngono. ^aAu "ni adilifu."

kweli huyu ni dada yangu, binti ya baba yangu lakini si binti ya mama yangu, naye akawa mke wangu.^a **13** Kwa hiyo Mungu aliponifanya nita- ngetange kutoka katika nyumba ya baba yangu,^b nilimwambia mke wangu: ‘Hivi ndivyo utakavyonionyesha upendo mshikamanifu: Kila mahali tutakapokwenda, sema hivi kunihusu, “Huyu ni ndugu yangu.”’^c

14 Basi Abimeleki akachukua kondoo na ng’ombe na watumishi wa kiume na wa kike akampa Abrahamu, naye akamrudishia Abrahamu mke wake, Sara. **15** Pia Abimeleki akasema: “Tazama nchi yangu iko wazi mbele yako. Ishi popote unapopenda.” **16** Naye akamwambia Sara: “Tazama ninampa ndugu yako vipande 1,000 vya fedha.^d Ni ishara ya kwamba huna hatia* mbele ya wote walio pamoja nawe na mbele ya watu wote, nawe umeondolewa shutuma.” **17** Na Abrahamu akaanza kumwomba dua Mungu wa kweli, naye Mungu akamponya Abimeleki na mke wake na vijakazi wake, nao wakaanza kuzaa watoto; **18** kwa maana Yehova alikuwa amewafanya wanawake wote wa nyumba ya Abimeleki wawe tasa* kwa sababu ya Sara, mke wa Abrahamu.^e

21 Yehova akamkumbuka Sara kama alivyokuwa amesema, na Yehova akamtendea Sara jambo alilokuwa amemwahidi.^f **2** Basi

20:16 *Tnn., “Tazama, ni kifuniko cha macho kwako.” **20:18** *Au “alikuwa amefunga kabisa kila tumbo la uzazi la nyumba ya Abimeleki.”

SURA YA 20

a Mwa 11:29

b Mwa 12:1

c Mwa 12:13

d Mwa 20:2, 12

e Mwa 12:17

SURA YA 21

f Mwa 18:10

Safu ya 2

a Ebr 11:11

b Mwa 17:21
Mwa 18:10, 14
Ro 9:9

c Mwa 17:19
Yos 24:3
Ro 9:7

d Mwa 17:12
Law 12:3
Mdo 7:8

e Mwa 16:4, 15

f Mwa 15:13
Gal 4:22, 29

g Mwa 15:2, 4
Gal 4:30

h Mwa 17:18

Sara akapata mimba^a Abrahamu akiwa mzee, akamzaliamwana wakati uleule ambao Mungu alikuwa amemwahidi Abrahamu.^b **3** Abrahamu akamwita Isaka, mwana huyo ambaye Sara alikuwa amemzaliam.^c **4** Na Abrahamu akamta- hiri Isaka mwanawe akiwa na umri wa siku nane, kama Mungu alivyokuwa amemwamuru.^d **5** Abrahamu alikuwa na umri wa miaka 100 Isaka mwanawe alipozaliwa. **6** Kisha Sara akasema: “Mungu ameni- letea kicheko; kila mtu atakayesikia jambo hili atacheka pamoja nami.”* **7** Naye aka- ndelea kusema: “Ni nani ange- weza kumwambia Abrahamu, ‘Kwa hakika Sara atanyonye- sha watoto?’ Hata hivyo, ni- memzaliam mwana katika uzee wake.”

8 Basi mtoto huyo akakua na kuachishwa kunyonya, Abrahamu akafanya karamu kubwa siku ambayo Isaka aliachishwa kunyonya. **9** La- kini Sara alikuwa akiona kwa- mba mwana ambaye Hagari^e Mmisiri alimzaliam Abrahamu, alikuwa akimdhihaki Isaka.^f **10** Kwa hiyo akamwambia Abrahamu: “Mfukuze kijakazi huyu na mwanawe, kwa ma- ana mwana wa kijakazi huyu hatakuwa mrithi pamoja na mwanangu, pamoja na Isa- ka!”^g **11** Lakini jambo hilo alilomwambia Abrahamu ku- mhusu mwanawe, haliku- mpendeza kamwe Abrahamu.^h **12** Kisha Mungu akamwa- mbia Abrahamu: “Usikasiri- shwe na jambo ambalo Sara anakuambia kuhusu mvula- na huyo na kuhusu kijakazi

21:6 *Au labda, “atanicheka.”

wako. Msikilize,* kwa maana ule utakaoitwa uzao wako utapitia[#] kwa Isaka.^a **13** Na kuhusu mwana wa kijakazi wako,^b nitatokeza pia taifa kutoka kwake,^c kwa sababu yeye ni uzao wako.”*

14 Basi Abrahamu akaamka asubuhi na mapema, aka-chukua mkate na kiriba cha ngozi chenye maji na kumpa Hagari. Akamtwika vitu hivyo begani na kumwambia aende zake pamoja na mwana-^d Kwa hiyo Hagari akaondoka na kutangatanga katika nyika ya Beer-sheba.^e **15** Mwishowe maji yaliyokuwa ndani ya kiriba hicho cha ngozi yakaisha, naye akamsukuma mvulana huyo chini ya kichaka fulani. **16** Kisha akaenda na kuketi chini peke yake, karibu umbali ambao mshale hufika unaporushwa kwa upinde, kwa maana alisema: “Sitaki kumwona mvulana huyu akifa.” Kwa hiyo akaketi chini umbali fulani na kuanza kulia kwa sauti na kutokwa na machozi.

17 Ndipo Mungu akasikia sauti ya mvulana huyo,^f na malaika wa Mungu akamwita Hagari kutoka mbinguni na kumwambia:^g “Hagari, kwa nini unalia? Usiogope, kwa sababu Mungu amesikia sauti ya mwanao pale alipo. **18** Simama, mwinue mwanao na umshike kwa mkono wako, kwa maana nitamfanya kuwa taifa kubwa.”^h **19** Kisha Mungu akamfungua macho, naye akaona kisima cha maji, akaenda na kukijaza maji kile ki-

21:12 *Tnn., “Isikilize sauti yake.”
[#]Tnn., “ile itakayoitwa mbegu yako itapitia.”
 21:13 *Tnn., “mbegu yako.”

SURA YA 21

a Mwa 17:19
 Ro 9:7
 Ebr 11:18

b Gal 4:22

c Mwa 16:9, 10
 Mwa 17:20
 Mwa 25:12, 16

d Mwa 25:5, 6

e Mwa 22:19

f Mwa 16:11

g Mwa 16:7, 8

h 1Nya 1:29-31

Safu ya 2

a Mwa 16:16

b Hes 10:12

c Mwa 20:17, 18
 Mwa 26:26, 28

d Mwa 20:14, 15

e Mwa 26:15, 20

riba cha ngozi na kumnywe-sha mwanawe. **20** Na Mungu alikuwa pamoja na mvulana huyo^a alipoendelea kukua. Aliishi nyikani, akawa mpi-ga mishale. **21** Alienda kui-shi katika nyika ya Parani,^b na mama yake akamtafutia mke kutoka katika nchi ya Misri.

22 Wakati huo Abimeleki akiwa pamoja na Fikoli mkuu wa jeshi lake akamwambia Abrahamu: “Mungu yuko pamoja nawe katika kila jambo unalofanya.”^c

23 Basi sasa niapie hapa mbele za Mungu kwamba hutanitendea kwa udanganyifu mimi na watoto wangu na wazao wangu, na kwamba utanitendea kwa upendo mshikamanifu mimi na wakaaji wa nchi ambayo umekuwa ukii-shi, kama nilivyokutendea kwa upendo mshikamanifu.”^d **24** Kwa hiyo Abrahamu akasema: “Ninaapa hivyo.”

25 Hata hivyo, Abrahamu akamlalamikia Abimeleki kuhusu kisima cha maji ambacho watumishi wa Abimeleki walikuwa wamechukua kwa nguvu.^e **26** Abimeleki akamwambia: “Sijui ni nani aliyefanya jambo hilo; hukuniambia jambo hilo, leo ndio ninasikia habari hizo.”

27 Ndipo Abrahamu akachukua kondoo na ng’ombe na kumpa Abimeleki, na wote wawili wakafanya agano. **28** Abrahamu alipowatenga wanakondoo jike saba kutoka katika kundi, **29** Abimeleki akamuuliza Abrahamu: “Kwa nini umewatenga hawa wanakondoo jike saba?” **30** Akamjibu: “Pokea hawa wanakondoo jike saba kutoka mkononi mwangu kama ushahidi

kwamba mimi ndiye niliyechimba kisima hiki.” **31** Ndiyo maana alipaita mahali hapo Beer-sheba,*^a kwa sababu wote wawili walikuwa wamekula kiapo mahali hapo. **32** Kwa hiyo wakafanya agano^b huko Beer-sheba, kisha Abimeleki akaondoka pamoja na Fikoli mkuu wa jeshi lake, wakarudi katika nchi ya Wafilisti.^c **33** Baada ya hayo Abrahamu akapanda mti wa mwesheli huko Beer-sheba, na huko akalitia jina la Yehova,^d Mungu wa milele.^e **34** Naye Abrahamu akaishi* katika nchi ya Wafilisti kwa muda mrefu.^{#f}

22 Sasa baada ya mambo hayo Mungu wa kweli akamjaribu^g Abrahamu, akamwambia: “Abrahamu!” akajibu: “Mimi hapa!” **2** Kisha Mungu akamwambia: “Tafadhali, mchukue mwana wako, mwana wako wa pekee unayependa sana,^h Isaka,ⁱ usafiri kwenda katika nchi ya Moria/^j nawe umtoe kuwa dhabihu ya kuteketezwa juu ya mlima mmoja nitakaokuonyesha.”

3 Kwa hiyo Abrahamu akaamka asubuhi na mapema, akaweka matandiko juu ya punda wake na kuchukua wawili kati ya watumishi wake pamoja na Isaka mwanawe. Akapasua kuni kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa, kisha akafunga safari kwenda mahali ambapo Mungu wa kweli alimwonyesha. **4** Siku ya tatu, Abrahamu alinua macho, akapona mahali hapo kwa mbali. **5** Sasa Abraha-

21:31 *Labda inamaanisha “Kisima cha Kile Kiapo; Kisima cha Wale Saba.”
21:34 *Au “akaishi akiwa mgeni.”
#Tnn., “kwa siku nyingi.”

SURA YA 21

a Mwa 26:32, 33

b Mwa 26:26, 28

c Mwa 10:13, 14
Mwa 26:1

d Mwa 12:8, 9
Mwa 26:25

e Zb 90:2
Isa 40:28
1Ti 1:17

f Ebr 11:8, 9

SURA YA 22

g Ebr 11:17

h Yoh 3:16

i Mwa 17:19
Yos 24:3
Ro 9:7

j 2Nya 3:1

Safu ya 2

a Yoh 1:29
1Pe 1:18, 19

b Yoh 10:17, 18

c Ebr 11:17

d Ebr 11:17-19
Yak 2:21

mu akawaambia watumishi wake: “Ninyi kaeni hapa pamoja na punda, lakini mimi na mvulana huyu tutaenda kule ili kuabudu, halafu tutarudi.”

6 Kwa hiyo Abrahamu akachukua kuni kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa na kumtwika Isaka mwanawe. Halafu akabeba moto na kisu* mikononi, na wote wawili wakaendelea kutembea pamoja.

7 Kisha Isaka akamwambia Abrahamu baba yake: “Baba!” Akajibu: “Naam, mwanangu!” Halafu Isaka akauliza: “Hapa kuna moto na kuni, lakini yuko wapi kondoo kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa?”

8 Abrahamu akajibu: “Mwanangu, Mungu mwenyewe ataandaa kondoo kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa.”^a Na wote wawili wakaendelea kutembea.

9 Mwishowe wakafika mahali ambapo Mungu wa kweli alikuwa amemwonyesha, Abrahamu akajenga madhabahu hapo na kupanga kuni juu yake. Akamfunga Isaka mwanawe mikononi na miguu na kumlaza kwenye madhabahu juu ya zile kuni.^b **10** Kisha Abrahamu akaunyoosha mkono wake na kuchukua kisu* ili amuue mwanawe.^c

11 Lakini malaika wa Yehova akamwita kutoka mbinguni: “Abrahamu, Abrahamu!” naye akajibu: “Mimi hapa!” **12** Kisha akasema: “Usimdhuru mvulana huyu, wala usimtee lolote, kwa maana sasa ninajua kwamba unamwogopa Mungu kwa sababu hukuni-nyima^d mwana wako, mwana wako wa pekee.” **13** Ndipo

22:6, 10 *Au “kisu cha kuchinjia.”

Abrahamu akainua macho yake, na hapo karibu mbele yake kulikuwa na kondoo dume aliyenaswa kwa pembe zake kichakani. Kwa hiyo Abrahamu akaenda na kumchukua kondoo dume yuo na kumtoa dhabihu ya kuteketezwa badala ya mwanawe. **14** Naye Abrahamu akapaita mahali hapo Yehova-yire.* Ndiyo sababu mpaka leo inasemwa: "Katika mlima wa Yehova itaandaliwa."^a

15 Na malaika wa Yehova akamwita Abrahamu mara ya pili kutoka mbinguni, **16** akamwambia: "Naapa kwa nafsi yangu," asema Yehova,^b 'kwamba kwa kuwa umetenda jambo hili nawe hujaninyima mwana wako, mwana wako wa pekee,^c **17** hakika nitakubariki, nami hakika nitaufanya uzao* wako uwe mwingi kama nyota za mbinguni na kama chembe za mchanga kwenye ufuo wa bahari,^d na uzao* wako utamiliki lango la^e maadui wake.^e **18** Na kupitia uzao wako*^f mataifa yote ya dunia yatajipatia baraka kwa sababu umeisikiliza sauti yangu."^g

19 Baada ya hayo Abrahamu akarudi kwa watumishi wake, wakaondoka wote pamoja na kurudi Beer-sheba;^h na Abrahamu akaendelea kushi Beer-sheba.

20 Baadaye Abrahamu akaambiwa: "Tazama, Milka amemzalia pia Nahori ndugu yako i wana hawa: **21** Usi mzaliwa wake wa kwanza, Buzi ndugu yake, Kemueli baba ya Aramu,

22:14 *Maana yake "Yehova Ataandaa; Yehova Atahakikisha Jambo Hilo."
22:17 *Tnn., "mbegu." #Au "majiji ya."
22:18 *Tnn., "mbegu yako."

SURA YA 22

a Mwa 22:2
2Nya 3:1

b Ebr 6:13, 14

c Yoh 3:16
Ro 8:32
Ebr 11:17d Mwa 13:14, 16
Mwa 15:1, 5
Mdo 3:25e Zb 2:8
Da 2:44f Mwa 3:15
Ro 9:7
Gal 3:16

g Gal 3:8

h Mwa 21:31

i Mwa 11:26, 29

Safu ya 2

a Mwa 25:20

b Mwa 24:15
Ro 9:10

SURA YA 23

c Mwa 17:17

d Yos 14:15

e Mwa 35:27
Hes 13:22

f Mwa 12:5

g Mwa 10:15

h Mwa 17:1, 8
Ebr 11:9, 13

i Mwa 21:22

j 1Nya 1:13

22 Kesedi, Hazo, Pildashi, Yidlafu, na Bethueli."^a **23** Bethueli akamzaa Rebeka.^b Milka alimzalia Nahori ndugu ya Abrahamu wana hao wanane. **24** Suria wake, aliyeitwa Reuma, alimzalia pia wana hawa: Teba, Gahamu, Tahashi, na Maaka.

23 Na Sara aliishi miaka 127; hiyo ndiyo iliyokuwa miaka ya maisha ya Sara.^c **2** Basi Sara akafa huko Kiriath-arba,^d yaani, Hebroni,^e katika nchi ya Kanaani,^f naye Abrahamu akaanza kumwombolezea Sara na kumlilia. **3** Kisha Abrahamu akainuka na kutoka mahali ambapo maiti ya mke wake ilikuwepo, akawaambia wana wa Hethi:^g **4** "Mimi ni mgeni na mhamiaji miongoni mwenu.^h Nipeni ardhi ya kuzikia miongoni mwenu ili niweze kuwazika watu wangu waliokufa." **5** Ndipo wana wa Hethi wakamwambia Abrahamu: **6** "Tusikilize, bwana wetu. Wewe ni kiongozi aliyechaguliwa na Mungu* miongoni mwetu.ⁱ Unaweza kuwazika watu wako waliokufa mahali bora zaidi katika maeneo yetu ya kuzikia. Hakuna yeyote kati yetu atakayekunyima mahali pa kuwazika watu wako waliokufa."

7 Basi Abrahamu akasimama na kuinama mbele ya wenyewe wa nchi, wana wa Hethi,^j **8** akawaambia: "Ikiwa mme kubali nimzike mtu wangu aliyekufa, basi nisikilizeni na mumsihi Efroni mwana wa Zohari **9** aniuzie pango lake la Makpela; liko ukingoni mwa shamba lake. Na aniuzie

23:6 *Au labda, "kiongozi mkuu."

mbele yenu kwa kiasi kamili cha fedha^a ili niwe na mahali pa kuwazikia watu wangu.”^b

10 Sasa Efroni alikuwa ameketi kati ya wana wa Hethi. Kwa hiyo Efroni Mhiti akamjibu Abrahamu mbele ya wana wa Hethi, na mbele ya wote walioingia katika lango la jiji,^c akasema: **11** “Hapana, bwana wangu! Nisikilize. Ninakupa shamba hilo pamoja na pango lililomo. Nina-kupa mbele ya wana wa watu wangu. Mzike mtu wako aliyekufa.” **12** Ndipo Abrahamu akainama chini mbele ya wenyeji wa nchi **13** na kumwambia hivi Efroni mbele ya watu: “Tafadhali, nisikilize! Nitakupa kiasi kamili cha fedha kwa ajili ya shamba hilo. Zichukue kutoka mikononi mwangu, ili nimzike humo mtu wangu aliyekufa.”

14 Kisha Efroni akamwambia Abrahamu: **15** “Bwana wangu, nisikilize. Thamani ya shamba hili ni shekeli 400 za fedha,* lakini hiyo ni nini kati yangu na wewe? Mzike mtu wako aliyekufa.” **16** Abrahamu akamsikiliza Efroni, na Abrahamu akampimia Efroni kiasi cha fedha alichokuwa amemtajia mbele ya wana wa Hethi, shekeli 400 za fedha* kulingana na uzito uliokubaliwa na wafanyabiashara.^d **17** Kwa hiyo shamba la Efroni lililokuwa Makpela, mbele ya Mamre—shamba na pango lililokuwemo na miti yote iliyokuwa ndani ya mipaka ya shamba hilo—likathibitishwa kuwa **18** mali ya Abrahamu aliyoinunua mbe-

23:15, 16 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 23

a Mwa 23:15

b Mwa 25:9, 10
Mwa 49:29-33
Mwa 50:13, 14

c Ru 4:1

d Mdo 7:15, 16

Safu ya 2

a Mwa 25:9, 10
Mwa 49:29-33
Mwa 50:13, 14

SURA YA 24

b Mwa 13:2

c Mwa 15:2, 3

d Mwa 28:1
Kum 7:1, 3
2Ko 6:14

e Mwa 22:20-23

f Mwa 11:27, 28
Mwa 15:7

g Ebr 11:15

h Mwa 12:1
Ebr 11:8

i Mik 7:20
Lu 1:72, 73
Ebr 6:13, 14

le ya wana wa Hethi, mbele ya wote walioingia katika lango la jiji lake. **19** Baada ya hayo Abrahamu akamzika Sara mke wake katika pango la shamba la Makpela mbele ya Mamre, yaani, Hebroni, katika nchi ya Kanaani. **20** Hivyo wana wa Hethi wakamkabidhi Abrahamu lile shamba pamoja na pango lililokuwemo ili awazike watu wake humo.^a

24 Sasa Abrahamu alikuwa amezeeka, umri wake ulikuwa umesonga, na Yehova alikuwa amembariki Abrahamu katika kila jambo.^b **2** Abrahamu akamwambia mtumishi wake, aliye-kuwa na umri mkubwa zaidi nyumbani mwake, ambaye alisimamia mali zake zote:^c “Tafadhali, weka mkono wako chini ya paja langu, **3** nami nitakuapisha kwa jina la Yehova, Mungu wa mbingu na Mungu wa dunia, kwamba hutamchukulia mwanangu mke kutoka kwa mabinti wa Wakanaani, ninaoishi miongoni mwa.^d **4** Badala yake unapaswa kwenda katika nchi yangu na kwa watu wangu wa ukoo,^e ukamchukulie mke mwanangu Isaka.”

5 Lakini mtumishi huyo akamuuliza: “Namna gani mwanamke huyo akikataa kuja pamoja nami katika nchi hii? Je, nimrudishe mwana wako katika nchi uliyotoka?”^f

6 Ndipo Abrahamu akamwambia: “Hakikisha kwamba humpeleki mwanangu huko.^g

7 Yehova Mungu wa mbinguni, aliyenitoa katika nyumba ya baba yangu na kutoka katika nchi ya watu wangu wa ukoo^h na ambaye alizungumza nami na kuniapia:ⁱ ‘Nitau-

pa uzao wako*^a nchi hii,^b atamtuma malaika wake mbele yako,^c nawe hakika utamchukulia mwanangu mke kutoka huko.^d **8** Lakini ikiwa mwanamke huyo atakataa kuja pamoja nawe, utakuwa huru kutokana na kiapo hiki. Lakini usimpeleke mwanangu huko.” **9** Ndipo mtumishi huyo akaweka mkono wake chini ya paja la Abrahamu bwana wake na kumwambia kuhusu jambo hilo.^e

10 Basi mtumishi huyo akachukua ngamia kumi kati ya ngamia wa bwana wake na kuondoka, akiwa na vitu vizuri vya kila aina kutoka kwa bwana wake. Kisha akaenda zake Mesopotamia, katika jiji la Nahori. **11** Akawapumzisha ngamia* kwenye kisima cha maji kilichokuwa nje ya jiji. Ilikuwa inaelekea jioni, wakati ambapo wanawake huenda kisimani kuteka maji. **12** Kisha akasema: “Yehova Mungu wa bwana wangu Abrahamu, tafadhali, nifanikishe leo, na umtendee kwa upendo wako mshikamanifu bwana wangu Abrahamu. **13** Nimesimama hapa kwenye chemchemi ya maji, na mabinti wa watu wa jiji wanakuja kuteka maji. **14** Na itukie kwamba msichana nitakayemwambia, ‘Tafadhali, ushushe mtungi wako ili ninywe maji,’ naye aseme, ‘Kunywa, nami nitawanywesha ngamia wako pia,’ na awe ndiye uliyemchagulia mtumishi wako, Isaka; na kwa jambo hilo acha nijue kwamba umemtendea bwana wangu kwa upendo wako mshikamanifu.”

24:7 *Tnn., “mbegu yako.” 24:11 *Tnn., “Akawapigisha magoti ngamia.”

SURA YA 24

a Ebr 11:18

b Mwa 13:14, 15
Mwa 26:3, 4
Kum 34:4
Mdo 7:4, 5

c Ebr 1:7, 14

d Mwa 12:5

e Mwa 24:2, 3

Safu ya 2

a Mwa 22:23

b Mwa 11:29

c Mwa 11:26

15 Hata kabla hajamaliza kuongea, Rebeka, binti ya Bethueli^a mwana wa Milka^b mke wa Nahori,^c ndugu ya Abrahamu, akaja akiwa amebeba mtungi wa maji begani. **16** Basi msichana huyo alikuwa mrembo sana, bikira; hakuna mwanamume yeyote aliyekuwa amefanya ngono naye. Akateremka chini kwenye chemchemi, akaujaza maji mtungi wake, kisha akapanda kurudi. **17** Mara moja yule mtumishi akakimbia ili akutane naye, akamwambia: “Tafadhali, nipe maji kidogo ninywe kutoka kwenye mtungi wako.” **18** Msichana huyo akasema: “Kunywa, bwana wangu.” Ndipo akaushusha haraka mtungi wake na kushikilia ili anywe maji. **19** Alipomaliza kumpa maji ya kunywa, akasema: “Nitateka pia maji kwa ajili ya ngamia wako mpaka watosheke.” **20** Kwa hiyo akamimina haraka maji ya mtungi wake ndani ya chombo cha kuwanywesha wanyama, naye akakimbia tena na tena kisimani kuteka maji, akaendelea kuteka maji kwa ajili ya ngamia wake wote. **21** Wakati huo wote mwanamume huyo alikuwa kimya akimtaazama kwa mshangao, akijiuliza kama Yehova alikuwa amefanikisha safari yake au la.

22 Ngamia walipotosheka kunywa maji, mwanamume huyo akatoa na kumpa pete ya puani ya dhahabu yenye uzito wa nusu shekeli* na bangili mbili za dhahabu zenye uzito wa shekeli kumi,*

24:22 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

23 kisha akamuuliza: “Tafadhali niambie, wewe ni binti ya nani? Kuna nafasi katika nyumba ya baba yako ambamo tunaweza kulala usiku huu?” **24** Akamjibu: “Mimi ni binti ya Bethueli^a mwana wa Milka, ambaye alimzalia Nahori.”^b **25** Akaendelea kusema: “Tuna nyasi na chakula kingi cha mifugo na pia mahali mnapoweza kulala usiku.” **26** Ndipo mwanamume huyo akainama chini na kusujudu mbele za Yehova **27** na kusema: “Yehova na asifiwe, Mungu wa bwana wangu Abrahamu, kwa maana hajaacha kumtendea bwana wangu kwa upendo wake mshikamanifu na kwa uaminifu wake. Yehova ameniongoza mpaka kwenye nyumba ya ndugu za bwana wangu.”

28 Kisha msichana huyo akakimbia kuwaambia watu wa nyumbani mwa mama yake kuhusu mambo hayo. **29** Sasa Rebeka alikuwa na ndugu aliyeitwa Labani.^c Basi Labani akakimbia kwenda kukutana na huyo mwanamume aliyekuwa nje kwenye chemchemi. **30** Labani alipoona ile pete na zile bangili mikononi mwa dada yake na kuyasikia maneno ya Rebeka dada yake, ambaye alikuwa akisema, “Hivi ndivyo mwanamume huyo alivyoniambia,” Labani alikwenda kukutana na mwanamume huyo, ambaye bado alikuwa amesimama karibu na ngamia wake kando ya chemchemi. **31** Mara moja akamwambia: “Njoo, wewe uliyebarikiwa na Yehova. Kwa nini bado umesimama hapa nje? Nimekutayarishia nyumba na mahali kwa ajili

SURA YA 24

a Mwa 22:23

b Mwa 11:29

c Mwa 25:20
Mwa 29:10

Safu ya 2

a Mwa 15:2, 3

b Mwa 12:15, 16
Mwa 13:2
Mwa 24:1

c Mwa 21:1, 2
Ro 4:19
Ebr 11:11

d Mwa 25:5

e Mwa 24:2, 3
Mwa 28:1

f Mwa 22:20-23

g Mwa 24:4

h Mwa 24:5

i Mwa 48:15

j Ebr 1:7, 14

ya ngamia wako.” **32** Ndipo mwanamume huyo akaingia ndani ya nyumba, naye* akawafungua ngamia na kuwapa nyasi na chakula cha mifugo na kuleta maji ya kuosha miguu yake na miguu ya wanamume waliokuwa pamoja naye. **33** Hata hivyo, chakula kili-powekwa mbele yake, alisema: “Sitakula mpaka niwaambie kilichonileta.” Kwa hiyo Labani akamwambia: “Tuambie!”

34 Kisha akasema: “Mimi ni mtumishi wa Abrahamu.^a **35** Na Yehova amembariki sana bwana wangu, na amemtajirisha sana kwa kumpa kondoo na ng’ombe, fedha na dhahabu, watumishi wa kiume na wa kike, na ngamia na punda.^b **36** Isitoshе, Sara, mke wa bwana wangu, akiwa amezeeka,^c alimzalia bwana wangu mwana, na bwana wangu atampa kila kitu alichو nacho.^d **37** Kwa hiyo bwana wangu aliniapisha hivi: ‘Usimchukulie mwanangu mke kutoka kwa mabinti wa Wakanaani ambao ninaiishi katika nchi yao.^e **38** Hapana, bali utaenda katika nyumba ya baba yangu na katika ukoo wangu,^f nawe utamchukulia mwanangu mke kutoka huko.’^g **39** Lakini nikamuuliza bwana wangu: ‘Namna gani mwanamke huyo akikataa kuja pamoja nami?’^h **40** Akaniambia: ‘Yehova, ambaye nimetembea mbele zake,ⁱ atamtuma malaika wake/ pamoja nawe, naye hakika ataifanikisha safari yako, nawe utamchukulia mwanangu mke kutoka katika ukoo wangu na

24:32 *Huenda ni Labani.

kutoka katika nyumba ya baba yangu.^a **41** Utakuwa huru kutokana na kiapo chako ikiwa utaenda katika ukoo wangu nao wakatae kukupa msichana huyo. Hilo litakuweka huru kutokana na kiapo chako.^b

42 “Nilipofika kwenye chemchemi leo, nilisema: ‘Yehova Mungu wa bwana wangu Abrahamu, ikiwa utaitanikisha safari yangu, **43** nimesimama kwenye kisima. Itatukia kwamba msichana^c akija kuteka maji nitasema, “Tafadhali, niruhusu ninywe maji kidogo kutoka katika mtungi wako,”

44 naye ataniambia, “Kunywa maji, na pia nitateka maji kwa ajili ya ngamia wako.” Mwanamke huyo na awe ndiye ambaye Yehova amemchagulia mwana wa bwana wangu.’^d

45 “Kabla sijamaliza kusema maneno hayo moyoni mwangu, Rebeka akatokea akiwa amebeba mtungi begani, akateremka mpaka kwenye chemchemi na kuanza kuteka maji. Ndipo nikamwambia: ‘Tafadhali, nipe maji ninywe.’^e **46** Kwa hiyo akau-shusha haraka mtungi wake kutoka begani mwake, akasema: ‘Kunywa maji,^f nami nitawanyweshwa pia ngamia wako.’ Basi nikanywa maji, naye akawanyweshwa pia ngamia wangu. **47** Baada ya hayo nikamuuliza, ‘Wewe ni binti ya nani?’ akajibu, ‘Binti ya Bethueli mwana wa Nahori, ambaye Milka alimzalia.’ Kwa hiyo nikamvisha pete puani na bangili mikononi mwake.^g

48 Nami nikainama chini na kusujudu mbele za Yehova na kumsifu Yehova Mungu wa bwana wangu Abrahamu,^h ali-

SURA YA 24

a Mwa 11:25

b Mwa 24:9

c Mwa 24:16

d Mwa 24:14

e Mwa 24:15, 17

f Mwa 24:18

g Mwa 24:22, 23

h Mwa 24:27

Safu ya 2

a Mwa 24:8

yekuwa ameniongoza kwenye njia inayofaa ili nimchukue binti ya ndugu ya bwana wangu kwa ajili ya mwana wake.

49 Na sasa niambieni ikiwa mnataka kumtendea bwana wangu kwa upendo mshikamanifu na uaminifu; lakini ikiwa sivyoy, niambieni, ili nijue jambo la kufanya.”^{*a}

50 Ndipo Labani na Bethueli wakajibu: “Jambo hili limetoka kwa Yehova. Hatuwezi kukuambia ndio au la.*

51 Rebeka ndiye huyu hapa. Mchukue uende, na awe mke wa mwana wa bwana wako, kama Yehova alivyosema.”

52 Mtumishi wa Abrahamu aliposikia maneno yao, mara moja akainama chini kifudifudi mbele za Yehova. **53** Na mtumishi huyo akaanza kutoa vito vya fedha na dhahabu na mavazi na kumpa Rebeka, naye akampa ndugu yake na mama yake vitu vyenye thamani. **54** Kisha mtumishi huyo na wanaume waliokuwa pamoja naye wakalala na kunywa, nao wakalala huko usiku huo.

Alipoamka asubuhi alisema: “Niruhusuni niende kwa bwana wangu.” **55** Lakini ndugu na mama ya Rebeka wakamwambia: “Acha msichana huyu akae nasi kwa angalau siku kumi. Kisha anaweza kwenda.” **56** Lakini akawambia: “Msinicheleweshe, kwa maana Yehova ameifanikisha safari yangu. Niruhusuni niondoke, ili niende kwa bwana wangu.” **57** Kwa hiyo wakasema: “Acha tumwite msichana huyo tumuulize.”

24:49 *Tnn., “ili niende mkono wa kulia au wa kushoto.” **24:50** *Au “Hatuwezi kukuambia jambo jema au baya.”

58 Wakamwita Rebeka na kumuuliza: “Je, utakwenda na mtu huyu?” Akajibu: “Niko tayari kwenda.”

59 Basi wakamruhusu Rebeka^a dada yao na mlezi wake^{*b} waende pamoja na mtumishi wa Abrahamu na watu wake. **60** Nao wakambariki Rebeka na kumwambia: “Dada yetu, na uwe maelfu mara elfu kumi,* na uzao wako umiliki[#] lango la^Δ wale wanaowachukia.”^c **61** Kisha Rebeka na vijakazi wake wakainuka, wakapanda ngamia, na kumfuata mtumishi huyo. Kwa hiyo mtumishi huyo akamchukua Rebeka na kuondoka.

62 Sasa Isaka alikuwa ametoka upande wa Beer-lahai-roi,^d kwa maana alikuwa akiishi katika nchi ya Negebu.^e **63** Na Isaka alikuwa nje akitembea shambani akitafakari^f jioni giza linapokaribia kuingia. Alipoinua macho yake, tazama, aliona ngamia wakijal! **64** Rebeka alipoinua macho, alimwona Isaka, akashuka haraka kutoka kwenye ngamia. **65** Kisha akamuuliza mtumishi wa Abrahamu: “Mwanamume yule anayetembea shambani akija kutupokea ni nani?” Mtumishi huyo akajibu: “Ni bwana wangu.” Kwa hiyo Rebeka akachukua shela yake na kujifunika. **66** Na mtumishi huyo akamwambia Isaka mambo yote aliyokuwa amefanya. **67** Kisha Isaka akampeleka Rebeka ndani ya hema la Sara mama yake.^g Hivyo

24:59 *Yaani, mlezi wake ambaye sasa alikuwa kijakazi wake. **24:60** *Au “na uwe mama ya maelfu ya makumi ya maelfu.” #Tnn., “mbegu yako imiliki.” ^ΔAu “majiji ya.”

SURA YA 24

a Mwa 28:5

b Mwa 35:8

c Mwa 22:15, 17

d Mwa 16:14
Mwa 25:11

e Mwa 12:9
Mwa 20:1
Hes 13:22
Amu 1:9

f Zb 77:12
Zb 143:5

g Ebr 11:9

Safu ya 2

a Mwa 26:8

b Mwa 23:2, 19

SURA YA 25

c Mwa 37:28
Kut 2:15
Hes 31:2
Amu 6:2

d 1Nya 1:32, 33

e Mwa 24:36

f Mwa 21:14

g Mwa 23:8, 9
Mwa 49:29, 30

h Mwa 23:2, 19

akamchukua Rebeka, akawa mke wake; Isaka akampenda,^a akafarijika baada ya kifo cha mama yake.^b

25 Kisha Abrahamu akaoa mke mwingine, naye aliitwa Ketur. **2** Baada ya muda Ketur akamzalia Abrahamu watoto hawa: Zimrani, Yokshani, Medani, Midiani,^c Ishbaki, na Shua.^d

3 Yokshani akamzaa Sheba na Dedani.

Wana wa Dedani walikuwa Ashurimu, Letushimu, na Leumimu.

4 Wana wa Midiani walikuwa Efa, Eferi, Hanoki, Abida, na Eldaa.

Hao wote walikuwa wana wa Ketur.

5 Baadaye Abrahamu alimpa Isaka^e kila kitu alichokuwa nacho, **6** lakini Abrahamu akawapa zawadi wana wa masuria wake. Alipokuwa bado hai, akawaagiza waende upande wa mashariki, mbali na Isaka mwanawe,^f katika nchi ya Mashariki. **7** Abrahamu aliishi miaka 175. **8** Kisha Abrahamu akakata pumzi na kufa baada ya kuishi masha marefu, akiwa amezeeka na kuridhika, naye akazi kwa pamoja na watu wake.*

9 Isaka na Ishmaeli wanawe wakamzika katika pango la Makpela kwenye shamba la Efroni mwana wa Zohari Mhiti, lililo mbele ya Mamre,^g **10** shamba ambalo Abrahamu alinunua kutoka kwa wana wa Hethi. Abrahamu alizika huko pamoja na Sara mke wake.^h **11** Baada ya kifo cha

25:8 *Tnn., “akakusanywa kwa watu wake.” Huu ni msemo wa kishairi unao-rejelea kifo.

Abrahamu, Mungu aliendelea kumbariki Isaka mwanawe,^a na Isaka alikuwa akikaa kari-bu na Beer-lahai-roi.^b

12 Hii ndiyo historia ya Ishmaeli^c mwana wa Abrahamu ambaye Hagari^d Mmisri, kijakazi wa Sara, alimzalila Abrahamu.

13 Haya ndiyo majina ya wana wa Ishmaeli, kulingana na asili za koo zao: Nebayothi^e mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli, kisha Kedari,^f Adbeeli, Mibsamu,^g **14** Mishma, Duma, Masa, **15** Hadadi, Tema, Yeturi, Nafishi, na Kedema. **16** Hao ndio wana wa Ishmaeli, na hayo ndiyo majina yao kulingana na makao yao na kulingana na kambi zao,* wakuu 12 kulingana na koo zao.^h **17** Na Ishmaeli aliishi miaka 137. Kisha akakata punzi na kufa, naye akazikwa pamoja na watu wake.* **18** Nao wakaanza kuishi katika nchi ya Havilaⁱ karibu na Shuri,^j karibu na Misri, mpa-ka Ashuru. Aliishi karibu na ndugu zake wote.*^k

19 Na hii ndiyo historia ya Isaka mwana wa Abrahamu.^l

Abrahamu alimzaa Isaka. **20** Isaka alikuwa na umri wa miaka 40 alipomwoa Rebeka, binti ya Bethueli,^m Mwaramu wa Padan-aramu, dada ya Labani yule Mwaramu. **21** Naye Isaka akaendelea kumsihi Yehova kumhusu mke wake kwa sababu alikuwa tasa; kwa hiyo Yehova akasikiliza ombi lake, na Rebe-

25:16 *Au “kambi zao zilizozingirwa na kuta.” **25:17** *Tnn., “akakusanywa kwa watu wake.” Huu ni msemu wa kishairi unaorejelea kifo. **25:18** *Au labda, “Aliishi kwa uhasama na ndugu zake wote.”

SURA YA 25

a Mwa 17:19
Mwa 26:12-14

b Mwa 16:14

c Mwa 16:10, 11

d Gal 4:24

e Mwa 36:2, 3
Isa 60:7

f Zb 120:5
Yer 49:28
Eze 27:21

g 1Nya 1:29-31

h Mwa 17:20

i 1Sa 15:7

j Mwa 16:7, 8

k Mwa 16:11, 12

l Mwa 22:2
Mt 1:1, 2

m Mwa 22:23

Safu ya 2

a Ro 9:10

b Zb 139:15

c Mwa 36:31
Hes 20:14

d Mwa 27:29, 30
Kum 2:4

e 2Sa 8:14
Mal 1:2, 3
Ro 9:10-13

f Mwa 27:11

g Mwa 27:32
Mwa 36:9
Mal 1:3

h Ho 12:3

i Mwa 27:36

j Mwa 27:3, 5

k Ebr 11:9

l Mwa 27:6, 7, 46

ka mke wake akapata mimba. **22** Na wana waliokuwa tumboni mwake wakaanza kupambana,^a akasema: “Ikiwa hivi ndivyo mambo yali-vyo, kwa nini niendeleo kuisi-shi?” Basi akamuuliza Yehova kuhusu jambo hilo. **23** Yehova akamwambia: “Mataifa mawili yamo tumboni mwako,^b na mataifa mawili yatatengani-shwa kutoka ndani yako;^c na taifa moja litakuwa na nguvu kuliko lingine,^d na mkubwa atamtumikia mdogo.”^e

24 Wakati wake wa kuzaa ulipofika, tazama! mapacha walikuwa tumboni mwake. **25** Kisha wa kwanza akatoka, mwili wake wote ulikuwa mwekundu kama vazi la manyoya,^f kwa hiyo wakampa jina Esau.*^g **26** Kisha ndugu yake akatoka na mkono wake ulikuwa umeshika kisigino cha Esau,^h kwa hiyo akampa jina Yakobo.*ⁱ Isaka alikuwa na umri wa miaka 60 Rebeka alipowazaa.

27 Wavulana hao wali-poendelea kukua, Esau akawa mwindaji stadi,^j mtu wa mbugani, lakini Yakobo akawa mtu asiye na lawama, anayekaa katika mahe-ma.^k **28** Na Isaka alimpenda Esau kwa sababu alikuwa akimletea nyama za porini, lakini Rebeka alimpenda Yakobo.^l **29** Siku moja Yakobo alipokuwa akichemsha mchuzi, Esau alirudi kutoka mbugani akiwa amechoka. **30** Kwa hiyo Esau akamwambia Yakobo: “Fanya haraka, tafadhali,

25:25 *Maana yake “Mwenye Nywele Nyingi.” **25:26** *Maana yake “Anayeshika Kisigino; Anayechukua Nafasi ya Mwingine.”

nipe kiasi kidogo cha mchuzi huo mwekundu,* kwa maana nimechoka sana!"# Ndiyo sababu alipewa jina Edomu.^{Δa} **31** Ndipo Yakobo akamwambia: "Kwanza niuzie haki yako ya mzaliwa wa kwanza!"^b **32** Esau akasema: "Ninakaribia kufa! Haki ya kuzaliwa ina faida gani kwangu?" **33** Yakobo akamwambia: "Niapie kwanza!" Basi akamwapia na kumuuzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza.^c **34** Ndipo Yakobo akampa Esau mkate na mchuzi wa dengue, akala na kunywa, kisha akainuka na kwenda zake. Hivyo, Esau akaidharau haki yake ya kuzaliwa.

26 Sasa kulikuwa na njaa kali nchini, mbali na ile njaa kali ya kwanza iliyotokea siku za Abrahamu,^d kwa hiyo Isaka akaenda Gerari kwa Abimeleki mfalme wa Wafilisti. **2** Kisha Yehova akamtokea Isaka na kumwambia: "Usishuke kwenda Misri. Kaa katika nchi nitakayokuonyesha. **3** Kaa kama mgeni katika nchi hii,^e nami nitaendelea kuwa pamoja nawe na kukubariki kwa sababu nitakupa wewe na uzao wako* nchi zote hizi,^f nami nitatimiza kipo hiki nilichomwapia Abrahamu baba yako:^g **4** 'Nitaufanya uzao* wako uwe mwingi kama nyota za mbinguni;^h nami nitaupa uzao* wako nchi zote hizi;ⁱ na kupitia uzao* wako mataifa yote ya dunia yatajipatia baraka,^j **5** kwa sababu Abrahamu aliisikiliza

25:30 *Tnn., "chekundu, hiki chekundu." ^ΔAu "nina njaa kali." ^ΔMaana yake "Mwekundu." **26:3** *Tnn., "mbegu yako." **26:4** *Tnn., "mbegu."

SURA YA 25

- a Mwa 36:1
- b Kum 21:16, 17
- c Ebr 12:16

SURA YA 26

- d Mwa 12:10
- e Mwa 20:1
Ebr 11:8, 9
- f Mwa 12:7
Mwa 15:18
- g Mwa 22:16-18
Zb 105:9-11
Ebr 6:13, 14
- h Mwa 15:1, 5
Ebr 11:12
- i Kum 34:4
- j Mwa 12:1-3
Mdo 3:25
Gal 3:8

Safu ya 2

- a Mwa 17:10, 23
Mwa 22:3, 12
Ebr 11:8
Yak 2:21
- b Mwa 26:17
- c Mwa 12:11-13
- d Mwa 24:16
- e Mwa 24:67
- f Mwa 20:11
- g Mwa 12:18
- h Mwa 20:9

- i Mwa 24:34, 35

sauti yangu na kuendelea kuitii matakwa yangu, amri zangu, maagizo yangu, na sheria zangu."^a **6** Kwa hiyo Isaka akaendelea kuishi Gerari.^b

7 Wanaume wa huko wali-pomuuliza kuhusu mke wake, alikuwa akisema: "Huyu ni dada yangu."^c Aliogopa kusema, "Ni mke wangu," kwa kuwa alisema, "Huenda wanaume hawa wakaniua kwa sababu ya Rebeka," kwa maana alikuwa mrembo sana.^d

8 Baada ya muda kupita, Abimeleki mfalme wa Wafilisti alikuwa akiangalia nje dirishani, akamwona Isaka akimwonyesha mahaba* Rebeka mke wake.^e **9** Mara moja Abimeleki akamwita Isaka na kumwambia: "Kumbe ni mke wako! Mbona ulisema, 'Huyu ni dada yangu?'" Isaka akamwambia: "Nilisema hivyo kwa sababu niliogopa nita-uawa kwa sababu yake."^f

10 Lakini Abimeleki akamuuliza: "Ni jambo gani hili ulilotutendea?" Ingekuwa rahisi kwa yeyote kulala na mke wako, nawe ungetuletea hatia!"^h **11** Ndipo Abimeleki akawaamuru watu wote akisema: "Yeyote atakayemgusa mtu huyu na mke wake hakika atauawa!"

12 Na Isaka akaanza kupanda mbegu katika nchi hiyo, na mwaka huo alivuna mara 100 zaidi ya mbegu alizopanda, kwa kuwa Yehova alikuwa akimbariki.ⁱ **13** Mwanamume huyo akatajirika, naye akaendelea kupata ufanisi mpaka akawa tajiri sana. **14** Alipata makundi ya kondoo na makundi ya ng'o-

26:8 *Au "akimkumbatia."

mbe na kundi kubwa la watumishi,^a nao Wafilisti wakaanza kumwonea wivu.

15 Kwa hiyo Wafilisti wachukua udongo na kuvifukia visima vyote ambavyo watumishi wa baba yake walikuwa wamechimba siku za Abrahamu.^b **16** Kisha Abimeleki akamwambia Isaka: "Ondoka katika eneo letu, kwa sababu umekuwa na nguvu nyingi kuliko sisi." **17** Kwa hiyo Isaka akaondoka huko na kupiga kambi katika bonde* la Gerari^c na kuanza kuishi huko. **18** Na Isaka akavichimbua visima vilivyokuwa vimechimbwa katika siku za Abrahamu baba yake lakini ambavyo Wafilisti walivifukia baada ya Abrahamu kufa,^d akavipa majina yaleyale ambayo baba yake alivipa.^e

19 Watumishi wa Isaka walipokuwa wakichimba bonde ni,* walipata kisima cha maji safi. **20** Nao wachungaji wa Gerari wakaanza kugombana na wachungaji wa Isaka, wakisema: "Maji haya ni yetu!" Basi akakiita kisima hicho Eseki,* kwa sababu walikuwa wamegombana naye. **21** Nao wakaanza kuchimba kisima kingine, wakaanza kugombania pia. Basi akakiita Sitna.* **22** Baadaye akaondoka huko na kuchimba kisima kingine, lakini hawakugombania. Basi akakiita Rehobothi* na kusema: "Ni kwa sababu sasa Yehova ametupa nafasi ya kutosha naye ametufanya tuongezeke nchini."^f

26:17 *Au "korongo." **26:19** *Au "korongoni." **26:20** *Maana yake "Ugomvi." **26:21** *Maana yake "Shtaka." **26:22** *Maana yake "Maeneo Makubwa."

SURA YA 26

a Mwa 12:16

b Mwa 21:27, 30

c Mwa 10:19
Mwa 20:1

d Mwa 21:25

e Mwa 21:31

f Mwa 17:5, 6
Mwa 28:1, 3

Safu ya 2

a Mwa 21:31

b Mwa 17:1
Mwa 28:13

c Mwa 15:1

d Mwa 17:19
Zb 105:9-11

e Mwa 12:8, 9

f Ebr 11:9

g Mwa 21:32

h Mwa 21:22

i Mwa 21:27

j Mwa 21:22-24

k Mwa 26:18

23 Kisha akapanda kutoka huko na kwenda Beer-sheba.^a

24 Yehova akamtokea usiku huo na kumwambia: "Mimi ni Mungu wa Abrahamu baba yako.^b Usiogope,^c kwa maana niko pamoja nawe, nami nitakubariki na kufanya uzao* wako uwe mwingi kwa sababu ya Abrahamu mtumishi wangu."^d **25** Basi akajenga madhabahu huko na kuliitia jina la Yehova.^e Na Isaka akapiga hema lake huko,^f na watumishi wake wakachimba kisima huko.

26 Baadaye Abimeleki akamtembelea kutoka Gerari akiwa pamoja na Ahuzathi mshauri wake na Fikoli mkuu wa jeshi lake.^g **27** Basi Isaka akawauliza: "Kwa nini mmenitembelea, ilhali mlinichukia na kunifukuza katika eneo lenu?" **28** Wakamwambia: "Tumeona wazi kwamba Yehova amekuwa pamoja nawe.^h Basi tukasema, 'Tafadhali, na kuwe na kiapo cha wajibu kati yetu sisi na wewe, na tufanye agano pamoja nawe'ⁱ **29** kwamba hutatutendea jambo lolote baya kama vile ambavyo hatujakudhuru, kama ujuavyo tulikutendea mema tu na tulikuruhusu uende zako kwa amani. Sasa wewe ni mbarikwi wa Yehova."^j **30** Kisha akawafanyia karamu, nao wakala na kunywa. **31** Asubuhi wakaamka mapema na kufanya kiapo kati yao.^j Kisha Isaka akawaruhusu waende zao, nao wakaondoka kwa amani.

32 Siku hiyo watumishi wa Isaka walikuja na kumwambia kuhusu kisima walichokua wamechimba,^k wakasema:

26:24 *Tnn., "mbegu."

“Tumepata maji!” **33** Kwa hiyo akakiita Shiba. Ndiyo sababu tangu siku hiyo jiji hilo linaitwa Beer-sheba.^a

34 Esau alipokuwa na umri wa miaka 40, alimwoa Yudithi binti ya Beeri Mhiti na pia Basemathi binti ya Eloni Mhiti.^b **35** Walikuwa chanzo cha huzuni kubwa* kwa Isaka na Rebeka.^c

27 Sasa Isaka alipozeeka na macho yake yalipokuwa yamedhoofika sana asiweze kuona, alimwita Esau^d mwanawe mkubwa na kumwambia: “Mwanangu!” Naye akamjibu: “Naam, babal!” **2** Isaka akamwambia: “Sasa nimezeeka. Sijui nitakufa lini. **3** Basi sasa hivi, tafadhali, chukua silaha zako, podo lako na upinde wako, uende mbugani ukaniwindie mnyama wa mwituni.^e **4** Kisha unipikie chakula kitamu ninachokipe nda sana. Nami nitakila ili nikubariki kabla sijafa.”

5 Hata hivyo, Rebeka alikuwa akisikiliza Isaka alipokuwa akizungumza na Esau mwanawe. Kisha Esau akaenda mbugani kuwinda mnyama wa mwituni na kumleta.^f **6** Basi Rebeka akamwambia Yakobo mwanawe:^g “Nimetoka kumsikia baba yako akizungumza na ndugu yako Esau na kumwambia, **7** Nilettee nyama ya porini, unipikie chakula kitamu. Kisha unipe nile ili nikubariki mbele za Yehova kabla sijafa.”^h **8** Na sasa, mwanangu, sikiliza kwa makini na ufanye ninayokuagiza.ⁱ **9** Tafadhali, nenda kundini unilettee wanambuzi wawili walio

26:35 *Tnn., “uchungu mkali wa rohani.”

SURA YA 26

a Amu 20:1

b Mwa 36:2, 3

c Mwa 27:46
Mwa 28:8

SURA YA 27

d Mwa 25:28

e Mwa 25:27

f Mwa 27:30

g Mwa 25:28

h Mwa 27:30, 31

i Mwa 27:13, 43

Safu ya 2

a Mwa 25:25
Mwa 27:23

b Mwa 27:21

c Mwa 27:8, 43

d Mwa 25:23, 26

e Mwa 25:25
Mwa 27:11

f Mwa 27:9

g Mwa 25:31-33
Ro 9:10-12

h Mwa 27:4

bora, ili nimpikie baba yako chakula kitamu, kama anavyopenda. **10** Kisha mpelekee baba yako ale, ili akubariki kabla hajafa.”

11 Yakobo akamwambia Rebeka mama yake: “Lakini Esau ndugu yangu ni mwanamume mwenye nywele nyingi,^a na ngozi yangu ni laini. **12** Itakuwaje baba akinigusa?^b Bila shaka ataona ninamdhihaki, nami nitajiletea laana badala ya baraka.” **13** Ndipo mama yake akamwambia: “Mwanangu, laana ambayo ingekupata na inipate mimi. Fanya tu ninayokwambia na uende, nilettee wanambuzi hao.”^c

14 Basi akaenda, akawachukua na kumletea mama yake, na mama yake akapika chakula kitamu, kama tu baba yake alivyopenda. **15** Baada ya hayo Rebeka akaingia nyumbani na kuchukua mavazi bora zaidi ya Esau mwanawe mkubwa, akamvisha Yakobo mwanawe mdogo.^d **16** Pia akamvisha ngozi za wanambuzi hao mikononi na pia kwenye sehemu isiyo na nywele shingoni.^e **17** Kisha akampa Yakobo mwanawe chakula kitamu alichopika na mkate aliokuwa ameoka.^f

18 Kwa hivyo akaingia kwa baba yake na kusema: “Baba!” naye akajibu: “Naam! Wewe ni nani, mwanangu?” **19** Yakobo akamwambia baba yake: “Mimi ni Esau mzaliwa wako wa kwanza.^g Nimefanya kama ulivyoniambia. Keti tafadhali, ule nyama niliyokupikia ili unibariki.”^h **20** Ndipo Isaka akamuuliza mwanawe: “Mwanangu, umepataje mawindo haraka sana hivyo?” Akajibu: “Ni kwa sababu Yehova Mu-

ngu wako aliniletea.” **21** Kisha Isaka akamwambia Yakobo: “Tafadhali mwanangu, karibia ili nikuguse, nijue ikiwa wewe kwa kweli ni mwanangu Esau au la.”^a **22** Kwa hiyo Yakobo akamkaribia Isaka baba yake, naye akamgusa, kisha akasema: “Sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau.”^b **23** Hakumtambua kwa sababu mikono yake ilikuwa na nywele nyingi kama mikono ya Esau ndugu yake. Kwa hiyo akambariki.^c

24 Kisha akamuuliza: “Je, kweli wewe ni mwanangu Esau?” akajibu: “Ni mimi.” **25** Halaflu akamwambia: “Mwanangu, niletee nyama ya porini nile, kisha nitakubariki.” Kwa hiyo akamletea, naye akala, pia akamletea divai, naye akanywa. **26** Kisha Isaka baba yake akamwambia: “Njoo karibu, tafadhali, unibusu, mwanangu.”^d **27** Kwa hiyo akakaribia na kumbusu, akasi- kisha harufu ya mavazi yake.^e Kisha akambariki na kusema:

“Tazama, harufu ya mwanangu ni kama harufu ya shamba ambalo Yehova amebariki. **28** Mungu wa kweli na akupe umande wa mbingu^f na udongo wenye rutuba duniani,^g na wingi wa nafaka na divai mpya.^h **29** Mataifa na yakutumikie, mataifa na yainame chini mbele yako. Uwe bwana juu ya ndugu zako, na wana wa mama yako na wainame chini mbele yako.ⁱ Alaa- niwe kila mtu anayekulaani, na abarikiwe kila mtu anayekubariki.”^j

30 Sasa Isaka alipomaliza tu kumbariki Yakobo na Yakobo alipotoka tu mbele ya Isaka baba yake, Esau ndu-

SURA YA 27

a Mwa 27:11, 12

b Mwa 27:16

c Ebr 11:20

d Mwa 48:10

e Mwa 25:27
Mwa 27:15

f Kum 11:11

g Hes 13:26, 27

h Mwa 27:37
Kum 7:13

i Mwa 25:23

j Mwa 12:1, 3
Mwa 28:1, 3
Mwa 31:42
Eze 25:12, 13

Safu ya 2

a Mwa 27:3

b Mwa 25:25, 31
Ebr 12:16

c Ebr 12:16, 17

d Mwa 25:26
Mwa 32:28
Ho 12:3

e Mwa 25:32-34

f Mwa 27:28

g Mwa 25:23
Mwa 27:29
Ro 9:10, 12

h Kum 33:28

gu yake akarudi kutoka mawindoni.^a **31** Yeye pia akapika chakula kitamu na kumletea baba yake, akamwambia baba yake: “Baba, amka ule nyama niliyokuletea, ili unibariki.” **32** Basi Isaka baba yake akamuuliza: “Wewe ni nani?” akamjibu: “Mimi ni mwana wako, mzaliwa wako wa kwanza, Esau.”^b **33** Kisha Isaka akaanza kutetemeka kwa nguvu sana, akasema: “Ni nani basi aliyewinda na kuniletea nyama? Tayari niliila kabla hujafika, nami nikambariki —naye hakika atabarikiwa!”

34 Aliposikia maneno ya baba yake, Esau akaanza kulia kwa sauti kubwa mno na kwa uchungu mwingi na kumwambia baba yake: “Nibariki mimi, naam, mimi pia, baba yangu!”^c **35** Lakini akamwambia: “Ndugu yako alikuja kwa udanganyifu ili apate baraka uliyopaswa kupata.” **36** Esau akamwambia: “Je, hiyo ndiyo sababu anaitwa Yakobo,^{*} ili achukue nafasi yangu mara mbili?”^d Tayari amechukua haki yangu ya mzaliwa wa kwanza,^e na sasa amechukua baraka yangu!”^f Kisha akauliza: “Hukuniachia baraka yoyote?” **37** Lakini Isaka akamjibu Esau: “Tazama, nimemweka awe bwana juu yako,^g nami nimempa ndugu zake wote wawe watumishi wake, nami nimempa nafaka na divai mpya ili kumtegemeza.^h Mwanangu, ni nini kilichobaki ninachoweza kukufanyia?”

38 Esau akamwambia baba yake: “Baba, je, una baraka moja tu? Nibariki mimi, naam,

27:36 *Maana yake “Anayeshika Kisigino; Anayechukua Nafasi ya Mwingine.”

mimi pia, baba yangu!” Ndipo Esau akalia kwa sauti kubwa na kububujikwa na machozi.^a **39** Basi Isaka baba yake akamwambia:

“Tazama, makao yako yatakuwa mbali na udongo wenyewe rutuba duniani, na mbali na umande wa mbingu.^b

40 Na kwa upanga wako utai-shi,^c nawe utamtumikia ndugu yako.^d Lakini utakaposhindwa kuvumilia, hakika utai-vunja nira yake kutoka shingoni mwako.”^e

41 Hata hivyo, Esau akawa na chuki kali dhidi ya Yakobo kwa sababu ya baraka ambayo baba yake alikuwa amempa,^f na Esau akawa akisema moyoni mwake: “Siku za kumwbolezea baba yangu zinakaribia.^g Zitakapokwisha nitamuua Yakobo ndugu yangu.” **42** Rebeka alipoambiwa maneno ya Esau mwana wake mku-bwa, mara moja akaagiza Yakobo mwana wake mdogo aitwe, akamwambia: “Tazama! Esau ndugu yako anapanga kukuua ili kulipiza kisasi.* **43** Sasa mwangu, fanya ninayokwambia. Ondoka, ukimbilie kwa Labani ndugu yangu kule Harani.^h **44** Ishi naye kwa muda mpaka ghadhabu ya ndugu yako itulie, **45** mpaka hasira ambayo ndugu yako anayo kukuelekea ipungue, naye asahau mambo uliyomtendea. Kisha nituma ujumbe ili urudi kutoka huko. Kwa nini niwapoteze nyote wawili siku moja?”

46 Baada ya hayo Rebeka akawa akimwambia Isaka: “Ni-

27:42 *Au “anajifariji kwa mawazo ya kukuua.”

SURA YA 27

a Ebr 12:16, 17

b Yos 24:4
Ebr 11:20

c Mwa 32:6
Hes 20:18

d Mwa 25:23
2Sa 8:14
Mal 1:2, 3

e 2Fa 8:20
2Nya 28:17

f Amo 1:11

g Mwa 35:28, 29

h Mwa 28:5

Safu ya 2

a Mwa 26:34, 35
Mwa 28:8

b Mwa 24:2, 3

SURA YA 28

c Mwa 24:34, 37
Kut 34:15, 16
1Fa 11:1-3
2Ko 6:14

d Mwa 29:16

e Mwa 17:5
Mwa 46:15, 19
1Nya 2:1, 2

f Mwa 12:2, 3

g Mwa 12:7
Mwa 15:13
Mwa 17:1, 8
Ebr 11:9

h Mwa 25:20

i Mwa 24:29

j Mwa 28:1
2Ko 6:14

k Mwa 27:43

l Mwa 27:46

nachukia maisha yangu kwa sababu ya mabinti wa Hethi.^a Yakobo akioa mke kutoka kwa mabinti wa Hethi, kama mabinti hawa wa nchi hii, maisha yangu yana faida gani?”^b

28 Basi Isaka akamwita Yakobo, akambariki na kumwamuru hivi: “Usioe mke kutoka kwa mabinti wa Kanaani.^c **2** Nenda Padan-aramu katika nyumba ya Bethueli, baba ya mama yako, na uoe mke kutoka kwa mabinti wa Labani,^d ndugu ya mama yako. **3** Mungu Mweza-Yote atakubariki na kukufanya uwe na wazao wengi na kuongezeka, nawe hakika utakuwa kusanyiko la mataifa.^e **4** Naye atakupua wewe na uzao wako* baraka ambayo alimwahidi Abrahamu,^f ili uimiliki nchi ambamo umekuwa ukiishi kama mgeni, nchi ambayo Mungu alimpa Abrahamu.”^g

5 Kwa hiyo Isaka akamruhusu Yakobo aondoke, naye akaenda Padan-aramu kwa Labani mwana wa Bethueli Mwaramu,^h ndugu ya Rebeka,ⁱ mama ya Yakobo na Esau.

6 Esau akaona kwamba Isaka alikuwa amambariki Yakobo na kumwambia aende Padan-aramu kuoia mke kutoka huko na kwamba alipambariki, alimwamuru, “Usioe mke kutoka kwa mabinti wa Kanaani.”^j **7** Na kwamba Yakobo alimtii baba yake na mama yake na kwenda Padan-aramu.^k **8** Ndipo Esau akatambua kwamba Isaka baba yake hakupendezwa na mabinti wa Kanaani,^l **9** kwa hiyo Esau akaenda kwa Ishmaeli

28:4 *Tnn., “mbegu yako.”

mwana wa Abrahamu na kumwoa Mahalathi binti ya Ishmaeli, dada ya Nebayothi, kuongezea wake wengine aliokuwa nao.^a

10 Yakobo akaondoka Beer-sheba na kuendelea na safari kuelekea Harani.^b **11** Baada ya muda akafika mahali fulani, akajitayarisha kulala hapo kwa sababu jua lilikuwa lime-tua. Kwa hiyo akachukua jiwe moja la mahali pale na kulikweka chini ili apumzisha kichwa chake juu yake, akalala hapo.^c **12** Kisha akaota ndoto, na tazama! Kulikuwa na ngazi iliyo-simamishwa duniani, na kilele chake kilifika mpaka mbinguni; na kulikuwa na malaika wa Mungu waliokuwa wakipanda na kushuka kwenye ngazi hiyo.^d **13** Na tazama! Yehova alikuwa amesimama juu yake, naye akasema:

“Mimi ni Yehova Mungu wa Abrahamu baba yako na Mungu wa Isaka.^e Nchi unayoi-lalia, nitakupa wewe na uzao wako.^f **14** Na hakika uzao wako utakuwa kama che-mbe za mavumbi ya ardhi,^g nawe utaenea mpaka upande wa magharibi na upande wa kaskazini na upande wa kusini, na kupitia kwako na kupitia uzao wako familia zote duniani hakika zitabarikiwa.^h **15** Niko pamoja nawe, nami nitakulinda popote utakapokwenda, nami nitakurudisha kwenye nchi hii.ⁱ Sitakuacha mpaka nitakapofanya mambo niliyokuahidi.”^j

16 Kisha Yakobo akaamka kutoka usingizini na kusema:

28:13 *Tnn., “mbegu yako.” **28:14** *Au “zitajipatia baraka.”

SURA YA 28

a Mwa 36:2, 3

b Mwa 11:31
Mwa 27:43

c Mwa 28:18, 19

d Yoh 1:51
Ebr 1:7, 14

e Mwa 26:24, 25

f Mwa 12:7
Mwa 28:4
Zb 105:9-11g Mwa 13:14, 16
1Fa 4:20h Mwa 18:18
Mwa 22:15, 18

i Mwa 35:6

j Mwa 31:3
Hes 23:19
Yos 23:14
Ebr 6:18

Safu ya 2

a Zb 47:2

b Mwa 35:1

c Mwa 31:13

d Mwa 35:6
Yos 16:1, 2

e Mwa 35:1

“Kwa kweli Yehova yuko mahali hapa, nami sikujua.” **17** Naye akaogopa na kusema: “Mahali hapa panaogopeshwa kwelikweli! Bila shaka hapa ni nyumba ya Mungu,^a na hili ndilo lango la mbingu.”^b **18** Kwa hiyo Yakobo akaamka asubuhi na mape-ma na kuchukua lile jiwe alilokuwa amepumzisha kichwa chake juu yake, akalisisimamisha kama nguzo na kumimina mafuta juu yake.^c **19** Basi akapaita mahali hapo Betheli,^{*} lakini hapo awali jiji hilo liliitwa Luzi.^d

20 Kisha Yakobo akaweka nadhiri hii: “Ikiwa Mungu ataendelea kuwa pamoja nami na kunilinda katika safari yangu na kunipa mkate wa kula na mavazi ya kuvaa **21** nami nirudi kwa amani katika nyumba ya baba yangu, kwa hakika Yehova atakuwa amethibitika kuwa Mungu wangu. **22** Na jiwe hili ambalo nimelisimamisha kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu,^e nami sitakosa kukupa sehemu ya kumi ya vitu vyote utakavyonipa.”

29 Baada ya hayo Yakobo akaendelea na safari yake, akafika katika nchi ya watu wa Mashariki. **2** Basi akaona kisima shambani na makundi matatu ya kondoo yakiwa yamelala kando yake, kwa sababu kwa kawaida wachungaji waliwanyweshwa kondoo wao maji ya kisima hicho. Kulikuwa na jiwe kubwa lililofunika kisima hicho. **3** Makundi yote ya kondoo yalipokusanywa hapo,

28:19 *Maana yake “Nyumba ya Mungu.”

wachungaji walilibingirisha jiwe lililofunika kisima hicho, nao wakawanywesha kondoo, kisha wakakifunika tena kisima kwa jiwe hilo.

4 Basi Yakobo akawauliza: “Ndugu zangu, mmetoka wapi?” wakamjibu: “Tumetoka Harani.”^a **5** Akawauliza: “Je, mnamjua Labani^b mjukuu wa Nahori?”^c wakamjibu: “Ndio, tunamjua.” **6** Ndipo akawauliza: “Je, hajambo?” wakamjibu: “Hajambo. Ndiye yule Raheli^d binti yake anakuja na kondoo!” **7** Kisha akasema: “Bado ni adhuhuri. Si wakati wa kukusanya kondoo. Wanwesheni kondoo, kisha wapelekeni malishoni.” **8** Wakawambia: “Haturuhusiwi kufanya hivyo mpaka maku ndi yote ya kondoo yakusanywe kisha jiwe libingirishwe kutoka juu ya kisima. Ndipo tutakapowanyesha kondoo.”

9 Alipokuwa akizungumza nao, Raheli akaja na kondoo wa baba yake, kwa maana alikuwa mchungaji. **10** Yakobo alipomwona Raheli binti ya Labani, ndugu ya mama yake, na kondoo wa Labani, mara moja Yakobo akakaribia na kulibingirisha jiwe linalofunika kisima, akawanywesha kondoo wa Labani ndugu ya mama yake. **11** Kisha Yakobo akambusu Raheli, akalika kwa sauti kubwa na kububujikwa na machozi. **12** Na Yakobo akaanza kumwambia Raheli kwamba yeye ni mtu wa ukoo wa* baba yake na kwamba yeye ni mwana wa Rebeka. Basi Raheli akakimbia na kwenda kumwambia baba yake.

29:12 * Tnn., “ndugu ya.”

SURA YA 29

a Mwa 27:42, 43
Mdo 7:2

b Mwa 24:29

c Mwa 24:24
Mwa 31:53

d Mwa 46:19
Ru 4:11

Safu ya 2

a Mwa 24:29

b Mwa 28:5

c Mwa 30:27, 28
Mwa 31:7

d Ru 4:11

e Mwa 31:41

f Mwa 30:26
Ho 12:12

13 Mara tu Labani^a aliposikia kuhusu Yakobo mwana wa dada yake, akakimbia kwenenda kumpokea. Akamkumbatia na kumbusu na kumleta nyumbani kwake. Naye akaanza kumwambia Labani mambo hayo yote. **14** Labani akamwambia: “Kwa kweli wewe ni mfupa wangu na nyama yangu.”* Basi akakaa naye kwa mwezi mzima.

15 Kisha Labani akamwambia Yakobo: “Je, unitumikie bure kwa sababu tu wewe ni mtu wangu wa ukoo?*”^b Niambie, ungependa mshahara wako uwe nini?”^c **16** Sasa Labani alikuwa na mabinti wawili. Yule mkubwa alitwa Lea, na mdogo alitwa Raheli.^d

17 Lakini macho ya Lea hayakuwa yaking’aa, lakini Raheli alikuwa mwanamke mwenye kuvutia sana, tena mrembo. **18** Yakobo alikuwa amempenda Raheli, kwa hiyo akasema: “Niko tayari kukutumikia kwa miaka saba ili nimpate Raheli binti yako mdogo.”^e

19 Labani akasema: “Ni afadhali nikupe wewe binti huyo kuliko kumpa mwanamume mwingine. Endelea kuka nama.” **20** Basi Yakobo akamtumikia Labani kwa miaka saba ili ampate Raheli,^f lakini machoni pake miaka hiyo ilikuwa kama siku chache tu kwa sababu ya upendo alikuwa nao kwa Raheli.

21 Kisha Yakobo akamwambia Labani: “Nipe mke wangu nilale naye kwa sababu siku zangu zimekwisha.” **22** Ndipo Labani akawakusanya wakaaji wote wa eneo hilo

29:14 * Au “mtu wangu wa ukoo niliye na uhusiano wa damu naye.” 29:15 * Tnn., “ndugu yangu?”

na kufanya karamu. **23** Lakin wakati wa jioni, akamchukua Lea binti yake na kumleta kwa Yakobo ili alale naye. **24** Pia, Labani akamchukua Zilpa kijakazi wake na kumpa Lea binti yake ili awe kijakazi wake.^a **25** Asubuhi Yakobo akagundua kwamba alipewa Lea! Kwa hiyo akamuuliza Labani: “Ni jambo gani hili ulilonitendea? Je, sikukutumikia ili nimpate Raheli? Kwa nini umenitendea hila?”^b **26** Labani akamjibu: “Si desturi yetu hapa kumwoza binti mdogo kabla ya yule aliyezaliwa kwanza. **27** Sherehekea juma la mwanamke huyu. Kisha utapewa mwanamke huyu mwingine ukinitumikia kwa miaka mingine saba.”^c **28** Yakobo akafanya hivyo, akashehekea juma la mwanamke huyu, kisha akampa Raheli binti yake awe mke wake. **29** Isitoshe, Labani alimchukua Bilha^d kijakazi wake na kumpa Raheli binti yake ili awe kijakazi wake.^e

30 Kisha Yakobo akalala pia na Raheli, naye alimpenda Raheli kuliko Lea, akamtumikia Labani kwa miaka mingine saba.^f **31** Yehova alipoonna kwamba Lea hapendwi,^{*} alimwezesha kupata mimba,^g lakini Raheli alikuwa tasa.^h **32** Kwa hiyo Lea akapata mimba na kuzaa mwana, akampa jina Rubeni,ⁱ kwa maana alisema: “Ni kwa sababu Yehova ameyaona mateso yangu,^j kwa maana sasa mume wangu ataanza kunipenda.” **33** Akapata mimba tena na kuzaa mwana, kisha akase-

29:31 *Tnn., “anachukiwa.” ^aTnn., “alifungua tumbo lake la uzazi.” 29:32 *Maana yake “Tazama, Mwana!”

SURA YA 29

a Mwa 16:1, 2
Mwa 30:9
Mwa 46:18

b Mwa 31:7, 42

c Mwa 31:41

d Mwa 35:22

e Mwa 30:1, 3

f Ho 12:12

g Mwa 46:15
Ru 4:11

h Mwa 30:22

i Mwa 35:22
Mwa 37:22
Mwa 49:3, 4
Kut 6:14
1Nya 5:1

j Mwa 30:20
1Sa 1:5, 6
Lu 1:24, 25

Safu ya 2

a Mwa 34:25
Mwa 49:5
1Nya 4:24

b Mwa 34:25
Mwa 49:5
Kut 6:16
Hes 3:12
1Nya 6:1

c Mwa 35:23
Mwa 37:26
Mwa 44:18
Mwa 49:8
1Nya 2:3
Ufu 5:5

SURA YA 30

d Mwa 29:29

e Mwa 35:22

f Mwa 35:25
Mwa 46:23
Mwa 49:16

ma: “Ni kwa sababu Yehova amesikiliza, kwa maana siku-pendwa, kwa hiyo amenipa huyu pia.” Basi akampa jina Simeoni.^{*a} **34** Akapata mimba tena na kuzaa mwana, kisha akasema: “Mara hii mume wangu ataungana nami, kwa sababu nimemzalia wana watatu.” Kwa hiyo mwana huyo akapewa jina Lawi.^{*b} **35** Akapata mimba tena na kuzaa mwana, akasema: “Wakati huu nitamsifu Yehova.” Kwa hiyo akampa jina Yuda.^{*c} Kisha akaacha kuzaa.

30 Raheli alipoona kwamba hajamzalia Yakobo watoto, alimwonea wivu dada yake, akaanza kumwambia Yakobo: “Nipe watoto, la sivyo nitakufa.” **2** Ndiyo hasira ya Yakobo ikawaka dhidi ya Raheli, akamwambia: “Je, nimechukua nafasi ya Mungu, ambaye amekuzaia kuzaa watoto?”^{*} **3** Raheli akamwambia: “Ndiye huyu kijakazi wangu Bilha.^d Lala naye ili anizalie watoto,^{*} na ili kupitia yeye, mimi pia nipate watoto.” **4** Basi akampa Bilha kijakazi wake awe mke wake, Yakobo akalala naye.^e **5** Bilha akapata mimba na baada ya muda akamzalia Yakobo mwana. **6** Raheli akasema: “Mungu amekuwa mwamuzi wangu, naye amesikiliza pia sauti yangu, akanipa mwana.” Ndiyo sababu alimpa jina Dani.^{*f} **7** Bilha, kijakazi wa Raheli,

29:33 *Maana yake “Kusikia.” 29:34 *Maana yake “Kushikamana; Ungana.” 29:35 *Maana yake “Aliyesifiwa; Kitu cha Kusifiwa.” 30:2 *Au “amekunyima uzao wa tumbo lako la uzazi?” 30:3 *Tnn., “azae kwenye magoti yangu.” 30:6 *Maana yake “Mwamuzi.”

akapata mimba tena na kumzalia Yakobo mwana wa pili. **8** Kisha Raheli akasema: “Nimepigana mieleka mikali sana na dada yangu. Na pia nimeibuka mshindi!” Kwa hiyo akampa jina Naftali.*^a

9 Lea alipoona kwamba ameacha kuzaa, alimchukua Zilpa kijakazi wake na kumpa Yakobo awe mke wake.^b

10 Na Zilpa kijakazi wa Lea akamzalia Yakobo mwana.

11 Kisha Lea akasema: “Kwa neema!” Basi akampa jina Gadi.*^c **12** Kisha Zilpa kijakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana wa pili. **13** Lea akasema: “Kwa furaha yangu! Kwa maana hakika mabinti watanitangaza kuwa mwenye furaha.”^d Basi akampa jina Asheri.*^e

14 Sasa Rubeni^f alikuwa akitembea siku za mavuno ya ngano, akapata dudai shambani. Kwa hiyo akamletea Lea mama yake. Basi Raheli akamwambia Lea: “Tafadhali, nipe baadhi ya dudai za mwana wako.” **15** Lea akamwambia: “Unafikiri ni jambo dogo kumchukua mume wangu?”^g Unataka pia kuchukua dudai za mwanangu?” Rahele akasema: “Ni sawa. Yakobo atalala nawe usiku wa leo ukinipa dudai za mwana wako.”

16 Yakobo alipokuwa akirudi kutoka shambani jioni, Lea alienda kumpokea, akamwambia: “Utalala nami kwa sababu nimekukodi kikamili kwa dudai za mwanangu.” Basi akalala naye usiku huo. **17** Na Mungu akamsikiliza

30:8 *Maana yake “Mieleka Yangu.”
30:11 *Maana yake “Neema.” **30:13** *Maana yake “Mwenye Furaha; Furaha.”

SURA YA 30

a Mwa 35:25
Mwa 46:24
Mwa 49:21
Kum 33:23

b Mwa 35:26

c Mwa 49:19
Hes 32:33

d Lu 1:46, 48

e Mwa 35:26
Mwa 46:17
Mwa 49:20
Kum 33:24

f Mwa 29:32

g Mwa 29:30

Safu ya 2

a Mwa 35:23
Mwa 46:13
Mwa 49:14
Kum 33:18

b Ru 4:11

c Mwa 29:32

d Mwa 35:23
Mwa 46:15
Zb 127:3

e Mwa 46:14
Mwa 49:13
Kum 33:18

f Mwa 34:1

g Mwa 29:31

h Lu 1:24, 25

i Mwa 35:24
Mwa 45:4
Kum 33:13
Mdo 7:9

j Mwa 28:15
Mwa 31:13

k Mwa 31:41
Ho 12:12

Lea na kumjibu, naye akapata mimba na baada ya muda akamzalia Yakobo mwana wa tano. **18** Kisha Lea akasema: “Mungu amenipa mshahara wangu* kwa sababu nimepema mume wangu kijakazi wangu.” Kwa hiyo akampa jina Isakari.*^a **19** Lea akapata mimba tena na baada ya muda akamzalia Yakobo^b mwana wa sita. **20** Lea akasema: “Mungu amenipa mimi zawadi, naam, amenipa mimi zawadi nzuri. Hatimaye, mume wangu atanivumilia,^c kwa maana nimemzalia wana sita.”^d Basi akampa jina Zabuloni.*^e **21** Baadaye akazaa binti na kumpa jina Dina.^f

22 Mwishowe Mungu akamkumbuka Raheli, na Mungu akamsikia na kumjibu kwa kumwezesha kupata mimba.*^g

23 Akapata mimba na kuzaa mwana. Akasema: “Mungu ameiondoa aibu yangu!”^h

24 Basi akampa mwana huyo jina Yosefu,*ⁱ akisema: “Yehova ananiongezea mwana mwingine.”

25 Baada ya Raheli kumzaa Yosefu, mara moja Yakobo akamwambia Labani: “Niruhusu niondoke ili niende nyumbani, katika nchi yangu.^j

26 Nipe wake zangu na watoto wangu, ambao nimekutumikia ili niwapate, niende zangu, kwa maana unajua vema jinsi nilivyokutumikia.”^k

27 Labani akamwambia: “Ikiwa nimepata kibali machoni

30:18 *Au “mshahara wa mtu aliyekodiwa.” ^aMaana yake “Yeye Ni Mshahara.” **30:20** *Maana yake “Kuvumilia.” **30:22** *Tnn., “na Mungu akamsikiliza na kufungua tumbo lake la uzazi.” **30:24** *Ufupisho wa jina Yosifia, linalomaanisha “Yah na Aongeze.”

pako,—ishara za ubashiri zimenisaidia* kuelewa kwamba Yehova ananibariki kwa sababu yako.” **28** Kisha akasema: “Niambie mshahara wako, nami nitakulipa.”^a **29** Basi Yakobo akamwambia: “Unajua jinsi nilivyokutumikia na jinsi nilivyoitunza mifugo yako;”^b **30** kabla sijaja ulikuwa na wanyama wachache, lakini sasa wameongezeka na kuwa wengi, naye Yehova amekubariki tangu nilipokuja. Basi nitaishughulikia lini nyumba yangu mwenyewe?”^c

31 Kisha akamuuliza: “Nikupe nini?” Yakobo akajibu: “Usinipe chochote! Lakini ukinifanyia jambo hili moja, nitaendelea kuichunga mifugo yako na kuilinda.”^d **32** Nitapita kati ya mifugo yako yote leo. Watenge kondoo wote wenye madoadoa na wenye mabakamabaka na kila mwanakondoo dume wa rangi ya kahawia na mbuzi jike yeyote mwenye madoadoa na mabakamabaka. Kuanzia sasa na kuendelea, watakuwa mshahara wangu.”^e **33** Na uadilifu* wangu utathibitisha kazi yangu siku utakapokuja kuangalia mshahara wangu; na ikiwa nitakuwa na mbuzi jike yeyote ambaye hatakuwa na madoadoa au mabakamabaka na mwanakondoo yeyote dume ambaye hatakuwa na rangi ya kahawia, basi atakuwa ameibwa.”

34 Labani akasema: “Vema! Na iwe kama ulivyosema.”^f

35 Basi siku hiyo akawatenga mbuzi dume wenye mistarimistari na mabakamaba-

30:27 *Au “mambo niliyoshuhudia yamenisaidia.” **30:33** *Au “unyooфу.”

SURA YA 30

a Mwa 31:7

b Mwa 31:38

c Mwa 32:9,10

d Ho 12:12

e Mwa 31:7

f Mwa 31:8

ka na mbuzi jike wote wenye madoadoa na mabakamabaka, na kila mwanakondoo dume mwenye madoadoa meupe na wa rangi ya kahawia; akawapa wanawe ili wawatunze. **36** Baada ya hayo Labani akasafiri kwa siku tatu kwenda kuchunga mifugo mbali na Yakobo, naye Yakobo akabaki akichunga mifugo ya Labani iliyosalia.

37 Ndipo Yakobo akachukua fito mbichi za mti wa mlubna, mlozi, na mwaramoni, akazibambua ili madoa meupe yaonekane. **38** Kisha akaziweka zile fito alizobambua mbele ya mifugo, kwenye mitaro, kwenye vyombo vya kunyweshea, mahali ambapo wanyama walikuja kunywa maji, ili wazione fito hizo na kupata joto la kupandana wanaopokuja kunywa maji.

39 Basi wanyama hao walipata joto na kupandana mbele ya fito hizo, nao walizaa wanyama wenye mistarimistari, madoadoa, na mabakamabaka. **40** Kisha Yakobo akawatenga wanakondoo dume, halafu akageuza wanyama wa Labani ili wawaangalie wanyama wenye mistarimistari na pia wanyama wote wa rangi ya kahawia kati ya mifugo ya Labani. Kisha akatenga mifugo yake, naye hakuichanganya na mifugo ya Labani. **41** Na kila mara wanyama wenye nguvu walipopata joto la kupandana, Yakobo aliweka zile fito kwenye mitaro ili wanyama hao wazione na kupata joto la kupandana. **42** Lakini wanyama walipokuwa dhaifu, hakuziweka fito hizo kwenye mitaro. Kwa hiyo

sikuzote wanyama dhaifu walikuwa wa Labani, lakini wenyewe nguvu walikuwa wa Yakobo.^a

43 Kwa hiyo Yakobo akatajirika sana, akawa na makundi makubwa ya wanyama na watumishi wa kiume na wa kike na ngamia na punda.^b

31 Baada ya muda Yakobo akawasikia wana wa Labani wakisema: “Yakobo amechukua kila kitu cha baba yetu, amepata utajiri huu wote kutokana na mali^c ya baba yetu.” **2** Kila mara Yakobo alipomtazama Labani, alitambua kwamba mtazamo wake kumwelekea ulikuwa umebadilika.^d **3** Hatimaye Yehova akamwambia Yakobo: “Rudi kwenye nchi ya baba zako na kwa watu wako wa ukoo,^e nami nitaendelea kuwa pamoja nawe.” **4** Kisha Yakobo akatuma ujumbe kwa Raheli na Lea na kuwaambia waje malishoni alikokuwa akichunga mifugo yake, **5** akawaambia:

“Nimeona kwamba mtazamo wa baba yenu kunielekea umebadilika,^f lakini Mungu wa baba yangu amekuwa pamoja nami.^g **6** Ninzi wenyewe mnajua kwa hakika kwamba nimemtumikia baba yenu kwa nguvu zangu zote.^h **7** Na baba yenu amejaribu kunidanganya na kubadili mshahara wangu mara kumi; lakini Mungu hajamruhusu anidhuru. **8** Kila mara aliposema, ‘Wanyama wenye madoadoa watakuwa mshahara wako,’ kundi lote lilizaa wanyama wenye madoadoa; na aliposema, ‘Wanyama wenye mistarimistari watakuwa mshahara

SURA YA 30

a Mwa 31:9

b Mwa 32:5
Mwa 36:6, 7

SURA YA 31

c Mwa 30:33

d Mwa 30:27

e Mwa 28:15
Mwa 32:9
Mwa 35:27

f Mwa 30:27

g Mwa 48:15

h Mwa 30:29, 30

Safu ya 2

a Mwa 30:32

b Mwa 30:39

c Mwa 29:25
Mwa 31:39

d Mwa 12:8, 9
Mwa 35:15

e Mwa 28:18, 22

f Mwa 35:14
Mwa 37:1

g Mwa 31:41
Ho 12:12

h Mwa 31:1

i Mwa 31:3

j Mwa 33:13

k Mwa 30:42, 43

wako,’ kundi lote lilizaa wanyama wenye mistarimistari.^a

9 Kwa hiyo Mungu akaendelea kuchukua mifugo ya baba yenu na kunipa. **10** Siku moja wanyama walipopata joto la kupandana, niliinua macho yangu na kuona katika ndoto kwamba mbuzi dume waliokuwa wakipanda majike walikuwa wenye mistarimistari, mabakamabaka, na madoadoa.^b **11** Kisha malaika wa Mungu wa kweli akaniita katika ndoto hiyo, ‘Yakobo!’ nikajibu, ‘Mimi hapa.’ **12** Akaniambia, ‘Tafadhali inua macho yako, uone kwamba mbuzi dume wote wanaowapanda majike wana mistarimistari, mabakamabaka, na madoadoa, kwa maana nimeona mambo yote ambayo Labani anakutendea.^c **13** Mimi ni Mungu wa kweli wa Betheli,^d mahali ambapo uliitia nguzo mafuta na kuniwekea nadhiri.^e Sasa inuka, ondoka katika nchi hii, urudi kwenye nchi uliyozaliwa.’”^f

14 Ndipo Raheli na Lea wakamuuliza: “Je, kuna urithi wowote uliobaki kwa ajili yetu katika nyumba ya baba yetu? **15** Je, haoni kwamba sisi ni wageni kwa sababu ametuuzi na amekuwa akitumia pesa alizopewa kwa ajili yetu?^g **16** Utajiri wote ambao Mungu amechukua kutoka kwa baba yetu ni wetu na wa watoto wetu.^h Basi sasa, fanya kila kitu ambacho Mungu amekuambia ufanye.”ⁱ

17 Kwa hiyo Yakobo akainuka na kuwapandisha watoto wake na wake zake juu ya ngamia,^j **18** naye akaanza kuchukua mifugo yake yote na mali zote alizokusanya^k huko

Padan-aramu, akaanza safari ya kwenda kwa Isaka baba yake katika nchi ya Kanaani.^a

19 Sasa Labani alikuwa ameenda kuwakata manyoya kondoo wake, Raheli akai-ba sanamu za terafimu*^b za baba yake.^c **20** Isitoshe, Yakobo akamshinda akili Labani, Mwaramu, kwa maana hakuwa amemwambia kwamba ataondoka. **21** Akatoroka na kuvuka ule Mto,^d yeye pamoja na vyote alivyokuwa navyo. Kisha akaelekea kwenye eneo lenye milima la Gileadi.^e **22** Siku ya tatu, Labani akaambiwa kwamba Yakobo ametoroka. **23** Basi Labani akawachukua ndugu zake* na kumfuatia Yakobo kwa muda wa siku saba na kumfikia katika eneo lenye milima la Gileadi. **24** Ndipo Mungu akamtokea Labani Mwaramu^f katika ndoto wakati wa usiku^g na kumwambia: “Uwe mwangalifu kuhusu mambo utakayomwambia Yakobo, yawe mema au mabaya.”^h

25 Basi Labani akamkaribia Yakobo alipokuwa amepiga hema lake mlimani; Labani alikuwa amepiga kambi na ndugu zake kwenye eneo lenye milima la Gileadi. **26** Labani akamuuliza Yakobo: “Umefanya nini? Kwa nini umenichezea akili na kuwachukua mabinti wangu kama mateka waliochukuliwa kwa upanga? **27** Kwa nini ulitoroka kwa siri, ukanichezea akili badala ya kuniambia? Ikiwa ungeniambia, ningekuaga kwa shangwe na nyimbo, kwa tari na kinubi. **28** Laki-

31:19 *Au “miungu ya familia; sanamu.” **31:21** *Yaani, Mto Efrati. **31:23** *Au “watu wake wa ukoo.”

SURA YA 31

a Mwa 35:27

b Mwa 35:2
Yos 24:2

c Mwa 31:14

d Mwa 15:18

e Hes 32:1

f Mwa 25:20
Ho 12:12

g Mwa 20:3

h Zb 105:15

Safu ya 2

a Mwa 31:24

b Mwa 31:19
Mwa 35:2

c Mwa 46:18, 25

ni hukunipa nafasi ya kuwabusu wajukuu* wangu na mabinti wangu. Umetenda kipumbavu. **29** Nina uwezo wa kuwadhuru, lakini Mungu wa baba yenu aliongea nami usiku wa kuamkia leo, akaniambia, ‘Uwe mwangalifu kuhusu mambo utakayomwambia Yakobo, yawe mema au mabaya.’^a **30** Sasa umeondoka kwa sababu umekuwa ukitamani sana kurudi kwenye nyumba ya baba yako, lakini kwa nini umeiba miungu yangu?”^b

31 Yakobo akamjibu Labani: “Ni kwa sababu niliogopa, kwa maana nilisema moyoni mwangu, ‘Huenda ukaniyang’anya kwa nguvu mabinti wako.’ **32** Yeyote utakayempata na miungu yako, atauawa. Pekua vitu nilivyo navyo mbele ya hawa ndugu zetu, uchukue chochote kilicho chako.” Lakini Yakobo hakujua kwamba Raheli alikuwa ameiba miungu hiyo. **33** Kwa hiyo Labani akaingia katika hema la Yakobo na hema la Lea na hema la wale vijakazi wawili,^c lakini hakuipata. Kisha akatoka katika hema la Lea na kuingia katika hema la Raheli. **34** Raheli alikuwa amechukua sanamu hizo za terafimu na kuziweka ndani ya kikapu cha wanawake kilicho kwenye matandiko ya ngamia na kuzikalia. Basi Labani alizitafuta kabisa katika hema lote lakini hakuzipata. **35** Ndipo Raheli akamwambia baba yake: “Bwanaangu, usikasirike, kwa sababu siwezi kusimama mbele yako, kwa maana niko katika siku

31:28 *Tnn., “wana.”

zangu za hedhi.”*^a Kwa hiyo akaendelea kuzitafuta kwa makini lakini hakuzipata sana mu hizo za terafimu.^b

36 Ndipo Yakobo akakasirika na kuanza kumshutumu Labani. Akamuuliza Labani: “Nimefanya kosa gani, nime-tenda dhambi gani hivi kwamba unanifuatia kwa bidii hivi? **37** Sasa kwa kuwa umepekua kabisa vitu vyangu vyote, umepata nini cha nyumba yako? Kiweke hapa mbele ya ndugu zangu na ndugu zako, waache waamue ni nani mwenye kosa kati yetu. **38** Kwa miaka hii 20 ambayo nimekaa nawe, mimba za kondoo wako na mbuzi wako hazikuharibika,^c wala sijawahi kula kondoo dume wa kundi lako. **39** Sijawahi kukuletea mnyama yeyote aliyeraruliwa na mnyama wa mwituni.^d Mimi mwenyewe nililipia hasara hiyo. Ulidai malipo kutoka kwangu kwa ajili ya mnyama yeyote aliyebiwa mchana au usiku. **40** Jua lilini-choma wakati wa mchana na baridi ilinipiga usiku, na mcho yangu yalipoteza usingizi.^e **41** Ilikuwa hivyo kwa miaka 20 niliyokaa nyumbani mwako. Nimekutumikia kwa miaka 14 ili niwapate mabinti wako wawili na kuchunga mifugo yako kwa miaka 6, nawe ulibadili tena na tena mshahara wangu mara kumi.^f **42** Ikiwa Mungu wa baba yangu,^g Mungu wa Abrahamu, Yule ambaye Isaka anamwogopa,^{*h} hangekuwa pamoja nami, sasa ungeniambia niende zangu mikono mitupu. Mungu ame-

31:35 *Tnn., “desturi ya wanawake ime-nijia.” 31:42 *Tnn., “woga wa Isaka.”

SURA YA 31

a Law 15:19

b Mwa 31:19

c Mwa 30:27

d 1Sa 17:34

e Mwa 47:9

f Mwa 31:7

g Mwa 28:13
Mwa 31:29

h Mwa 31:53

Safu ya 2

a Mwa 31:24

b Mwa 28:18

c Mwa 31:22, 23

yaona mateso yangu na kazi ngumu ya mikono yangu, na ndiyo sababu alikukaripia usiku wa kuamkia leo.”^a

43 Labani akamwambia Yakobo: “Mabinti hawa ni mabinti wangu na watoto hawa ni watoto wangu na wanyama hawa ni wanyama wangu, na kila kitu unachoona hapa ni changu na cha mabinti wangu. Ni jambo gani ninaloweza kufanya leo kuwadhuru mabinti hawa au kuwadhuru watoto wao ambao wame-wazaa? **44** Sasa njoo, tufanye agano kati yetu, wewe na mimi, nalo litakuwa ushahidi kati yetu.” **45** Basi Yakobo akachukua jiwe na kulisimamisha kama nguzo.^b **46** Kisha Yakobo akawaambia ndugu zake: “Okoteni mawe!” Basi wakaokota mawe na kutengeneza rundo la mawe. Halafu wakala chakula juu ya rundo hilo la mawe. **47** Na Labani akaanza kuliita rundo hilo Yegar-sahadutha,^{*} lakini Yakobo akaliita Galeedi.^c

48 Ndipo Labani akasema: “Rundo hili la mawe ni ushahidi kati yangu mimi na wewe leo.” Ndiyo sababu aliliita Galeedi,^c **49** na Mnara wa Mlinzi, kwa sababu alisema: “Yehova na awe mlinzi kati yangu mimi na wewe tunapokuwa hatuonani. **50** Ukiwatesa mabinti wangu na kuanza kuoa wake wengine kuongeza mabinti wangu, hata mwanaadamu asipoona jambo hilo, kumbuka kwamba Mungu atakuwa shahidi kati yangu mimi na wewe.” **51** Labani akaendelea kumwambia Yakobo:

31:47 *Neno la Kiaramu linalomaanisha “Rundo la Ushahidi.” [#]Neno la Kiebrania linalomaanisha “Rundo la Ushahidi.”

"Hili hapa ni rundo la mawe, na hii hapa ni nguzo ambayo nimesimamisha kati yangu mimi na wewe. **52** Rundo hili la mawe ni ushahidi, na nguzo hii pia ni ushahidi^a kwamba sitapita rundo hili la mawe ili kuja kukudhuru, nawe hutapita rundo hili la mawe na nguzo hii ili kuja kunidhuru. **53** Mungu wa Abrahamu^b na Mungu wa Nahori, Mungu wa baba yao, na awe mwamuzi kati yetu." Basi Yakobo akaapa kwa jina la Yule ambaye Isaka baba yake alimwogopa.*^c

54 Kisha Yakobo akatoa dhahibu mlimani na kuwaalika ndugu zake wale chakula.* Wakala na kulala mlimani usiku huo. **55** Hata hivyo, Labani akaamka asubuhi na mapema, akawabusu wajukuu wake^d na mabinti zake na kuwabariki.^e Kisha Labani akaondoka, akarudi nyumbani.^f

32 Kisha Yakobo akaendelea na safari yake, na malaika wa Mungu wakakutana naye. **2** Mara tu alipowaona, Yakobo akasema: "Hii ni kambi ya Mungu!" Kwa hiyo akapaita mahali hapo Mahanaimu.*

3 Kisha Yakobo akawatuma wajumbe wamtangulie kwenenda kwa Esau ndugu yake katika nchi ya Seiri,^g katika eneo* la Edomu,^h **4** akawaamuru hivi: "Hivi ndivyo mtakavyomwambia bwana wangu, Esau, 'Mtumishi wako Yakobo anasema hivi: "Nimeishi* na

31:53 *Tnn., "kwa woga wa Isaka baba yake." 31:54 *Tnn., "mkate." 32:2 *Maana yake "Kambi Mbili." 32:3 *Tnn., "shamba." 32:4 *Au "Nimeishi kama mgeni."

SURA YA 31

a Mwa 31:44, 45

b Mwa 17:1, 7

c Mwa 31:42

d Mwa 31:28

e Mwa 24:59, 60

f Mwa 27:43
Mwa 28:2

SURA YA 32

g Mwa 27:39
Mwa 36:8
Kum 2:5
Yos 24:4

h Mwa 25:30

Safu ya 2

a Mwa 31:41

b Mwa 30:43
Mwa 33:11

c Mwa 33:1, 2

d Mwa 27:41
Mwa 32:11

e Mwa 31:3, 13

f Mwa 28:15
Zb 100:5g Mwa 28:10
Mwa 30:43
Mwa 32:7

h Zb 34:4

i Mwa 27:41

Labani kwa muda mrefu mpaka sasa.^a **5** Nami nimepata ng'ombe dume, punda, kondoo, na watumishi wa kiume na wa kike,^b nami ninakutumia ujumbe huu bwana wangu, ili nipate kibali machoni pako."^c

6 Baada ya muda wajumbe hao wakarudi kwa Yakobo na kumwambia: "Tulikutana na ndugu yako Esau, naye yuko njiani, anakuja kukutana nawe akiwa na wanaume 400."^c **7** Ndipo Yakobo akao-gopa sana na kushikwa na wasiwasi.^d Basi akawagawa katika kambi mbili watu aliokuwa nao, na pia ng'ombe, ngamia, na mifugo mingine. **8** Akasema: "Esau akiishambulia kambi moja, kambi nyingine itaponyoka."

9 Kisha Yakobo akasema: "Ee Mungu wa baba yangu Abrahamu na Mungu wa baba yangu Isaka, Ee Yehova, wewe unayeniambia, 'Rudi kwenye nchi yako na kwa watu wako wa ukoo, nami nitakutendea mema,'^e **10** mimi si-stahili upendo wote mshikamanifu na uaminifu wote ambao umenitendea mimi, mtumishi wako,^f kwa maana nilivuka mto huu wa Yordani nikiwa na fimbo yangu tu lakini sasa nina kambi mbili.^g **11** Nakuomba uniokoe^h kutoka mikononi mwa ndugu yangu Esau, kwa maana naogopa kwamba anaweza kuja kunishambulia mimi,ⁱ na pia akina mama na watoto wao. **12** Lakini uliniambia: 'Hakika nitakutendea mema, nami nitaufanya uzao* wako uwe mwingi kama chembe za mchanga wa bahari,

32:12 *Tnn., "mbegu."

zisizoweza kuhesabiwa kwa sababu ni nyingi sana.”^a

13 Naye Yakobo akalala huko usiku huo. Kisha akachukua baadhi ya mali zake ili ampe zawadi Esau ndugu yake:^b **14** mbuzi jike 200, mbuzi dume 20, kondoo jike 200, kondoo dume 20, **15** ngamia 30 wanaonyonyesha, ng’ombe 40, ng’ombe dume 10, punda jike 20, na punda dume 10 waliokomaa.^c

16 Akawapa watumishi wake kundi moja baada ya lingine, akawaambia: “Nitangu-lieni mvuke kabla yangu, nanyi mwache nafasi kati ya kundi moja na kundi lingine.”

17 Pia akamwamuru hivi yule wa kwanza: “Ikiwa Esau ndugu yangu atakutana nawe na kukuuliza, ‘Wewe ni mtumishi wa nani, unaenda wapi, na wanyama hawa walio mbele yako ni wa nani?’ **18** utamwambia, ‘Ni mali ya mtumishi wako Yakobo. Ni zawadi aliyokutumia wewe, bwana wangu Esau,^d na tazama! yeye mwenyewe yuko nyuma anatumfuata.’” **19** Akamwamuru hivi pia mtumishi wa pili, wa tatu, na wale wote waliokuwa wakiyafuata makundi hayo: “Mkikutana na Esau, mtamwambia maneno hayo-hayo. **20** Vilevile mtamwambia, ‘Mtumishi wako Yakobo yuko nyuma anatumfuata.’” Kwa maana Yakobo alisema moyoni mwake: ‘Nikimtumia zawadi kwanza^e huenda nikamtuliza, na huenda atanipokea kwa fadhili nitakapokutana naye baadaye.’ **21** Kwa hiyo zawadi hizo zikavushwa na kupelekwa kwanza, lakini yeye mwenyewe akalala kam-bini usiku huo.

SURA YA 32

a Mwa 28:14
Mwa 46:2, 3
Kut 1:7
Kut 32:13
Mdo 7:17

b Mwa 33:10

c Mwa 30:43

d Mwa 33:8

e Mwa 43:11
1Sa 25:18

Safu ya 2

a Mwa 29:30
Ru 4:11

b Mwa 30:3, 9

c Kum 3:16
Yos 12:2
Amu 11:13

d Ho 12:3

e Mwa 32:31, 32

f Ho 12:4

g Mwa 35:10

h Ho 12:3

i Amu 13:17, 18

j 1Fa 12:25

k Mwa 16:7, 13
Amu 6:22
Yoh 1:18

22 Baadaye usiku huo, akaamka na kuwachukua wake zake wawili^a na vijakazi wake wawili^b na wanawe wachanga 11 na kuvuka kivuko cha Yaboki.^c **23** Basi akawachukua na kuwavusha kwenye kijito, * akavusha pia vitu vingine vyote alivyokuwa navyo.

24 Mwishowe Yakobo akabaki peke yake. Kisha mwana-mume fulani akaanza kupigana naye mweleka mpaka kulipopambazuka.^d **25** Mwana-mume huyo alipoona kwamba hajamshinda Yakobo, akamgusa kiungio cha nyonga; na kiungio cha nyonga ya Yakobo kikateguka alipokuwa akipigana naye mweleka.^e **26** Kisha mwanamume huyo akasema: “Niache niende, kwa maana kunapambazuka.” Yakobo akamwambia: “Sitakua-cha uende mpaka unibariki.”^f

27 Basi akamuuliza: “Jina lako ni nani?” akajibu: “Yakobo.” **28** Kisha akamwambia: “Jina lako halitakuwa tena Yakobo bali Israeli,^g *g kwa maana umepambana na Mungu^h na wanadamu na hatimaye umeshinda.” **29** Naye Yakobo akamuuliza: “Tafadhali, niambie jina lako.” Hata hivyo, mwanamume huyo akamwambia: “Kwa nini unataka kujua jina langu?”ⁱ Halafu akambariki huko. **30** Basi Yakobo akapaita mahali hapo Penieli,^{*j} kwa sababu alisema, “Nimemwona Mungu uso kwa uso, lakini uhai wangu umeokolewa.”^{*k}

32:23 *Au “bonde la mto; korongo.” **32:28** *Maana yake “Anayepambana na (Anayestahimili Pamoja na) Mungu” au “Mungu Hupambana.” **32:30** *Maana yake “Uso wa Mungu.” *Au “nafsi yangu imehifadhiwa.”

31 Na jua likachomoza mara tu Yakobo alipopita karibu na Penueli,* lakini alikuwa aki-chechemea kwa sababu ya nyonga yake.^a **32** Ndiyo maana tangu siku hiyo Waisraeli hawajazoea kula kano ya paja,* iliyo kwenye kiungio cha nyonga, kwa sababu mwanamume huyo aligusa kiungio cha nyonga ya Yakobo karibu na kano ya paja.

33 Sasa Yakobo akainua macho yake na kumwona Esau akija pamoja na wanaume 400.^b Kwa hiyo akawagawa watoto kati ya Lea, Raheli, na wale vijakazi wawili.^c **2** Akawaweka vijakazi na watoto wao mbele,^d kisha Lea na watoto wake,^e halafu Raheli na Yosefu nyuma yao. **3** Kisha yeye mwenyewe akaenda mbele yao, akainama mpaka chini mara saba huku akimkaribia ndugu yake.

4 Lakini Esau akakimbia kukutana naye, akamkumbatia na kumbusu, nao wakatoka na machozi. **5** Ali-poinua macho yake na kuona wanawake na watoto, akauliza: “Ni nani hawa walio pamoja nawe?” Yakobo akamwambia: “Ni watoto ambao Mungu amenipa kwa fadhili mimi mtumishi wako.”^g **6** Ndipo wale vijakazi wakaja mbele na watoto wao na kuinama chini, **7** Lea pia akaja mbele na watoto wake, nao wakainama chini. Kisha Yosefu akaja mbele na Raheli, nao wakainama chini.^h

8 Esau akauliza: “Msafara huu wote ni wa nini?”ⁱ Yakobo akamjibu: “Nimekuja ili ku-

32:31 *Au “Penieli.” 32:32 *Tnn., “kano ya mshipa wa paja.”

SURA YA 32
a Mwa 32:25

SURA YA 33
b Mwa 32:6

c Mwa 32:22

d Mwa 30:7,12

e Mwa 30:19

f Mwa 30:22-24

g Mwa 32:22
Zb 127:3

h Mwa 33:2

i Mwa 32:16

Safu ya 2

a Mwa 32:4, 5

b Mwa 36:6, 7

c Mwa 32:11, 20

d Mwa 32:13-15

e Mwa 30:43

f Mwa 31:17

g Mwa 32:3

h Yos 13:24, 27
1Fa 7:46

pata kibali machoni pako, bwana wangu.”^a **9** Esau akasema: “Nina mali nyingi sana, ndugu yangu.^b Usinipe mali zako.” **10** Lakini Yakobo akasema: “Hapana, tafadhali nakusihi. Ikiwa nimepata kibali machoni pako, pokea zawadi yangu kutoka mkononi mwangu, kwa sababu nimekuletea ili niuone uso wako. Nami nimeona uso wako kana kwamba nimeona uso wa Mungu, kwa maana umenipokea kwa furaha.^c **11** Tafadhali pokea zawadi yangu ya baraka uliyoletewa,^d kwa sababu Mungu amenibariki, nami nina kila kitu ninachohitaji.”^e Basi akaendelea kumsihi apokee zawadi hiyo, naye akai-chukua.

12 Baadaye Esau akasema: “Tuondoke, tufunge safari, acha nikutangulie.” **13** Lakini Yakobo akamwambia: “Bwana wangu unajua kwamba watoto ni dhaifu’ nami nina kondoo na ng’ombe wanaonyonyesha. Wakipeleka haraka-haraka kwa siku moja, wanyama wote wataku-fa. **14** Tafadhali, bwana wangu, nitangulie mimi mtumishi wako, lakini nitaendelea na safari polepole kulingana na mwendo wa mifugo na watoto mpaka nitakapofika kwa-ko bwana wangu huko Seiri.”^g **15** Esau akasema: “Tafadhali, naomba niwaache baadhi ya watu wangu pamoja nawe.” Yakobo akasema, “Kwa nini ufanye hivyo? Naomba tu nipate kibali machoni pako, bwana wangu.” **16** Basi siku hiyo Esau akasafiri kurudi Seiri.

17 Naye Yakobo akaenda Sukothi,^h naye akajijengea

nyumba na mabanda ya mifugo yake. Ndiyo sababu alipaita mahali hapo Sukothi.*

18 Baada ya kuondoka Padan-aramu,^a Yakobo akafika salama salimini kwenye jiji la Shekemu^b katika nchi ya Kanaani,^c naye akapiga kambi karibu na jiji hilo. **19** Kisha akanunua kisehemu fulani cha shamba kutoka kwa wana wa Hamori, baba ya Shekemu, kwa vipande 100 vya fedha, akapiga hema lake hapo.^d **20** Akajenga madhabahu huko na kuiita Mungu, Mungu wa Israeli.^e

34 Sasa Dina, binti ya Yakobo na Lea,^f alizoea kwenda kuwatembelea* mabinti wengine nchini.^g **2** Shekemu mwana wa Hamori Mhivi,^h mkuu wa nchi, alipomwona, alimchukua na kumbaka. **3** Shekemu akavutiwa sana na Dina binti ya Yakobo, akampenda msichana huyo na kuanza kumtongoza.* **4** Hatimaye Shekemu akamwambia Hamoriⁱ baba yake: “Nichukulia msichana huyu awe mke wangu.”

5 Yakobo aliposikia kwa mba Shekemu alikuwa amembaka Dina binti yake, wawe walikuwa na mifugo yake malishoni. Basi Yakobo akakaa kimya mpaka waliporudi. **6** Baadaye Hamori, baba ya Shekemu, akaja kuzungumza na Yakobo. **7** Lakini wana wa Yakobo wakasikia habari hizo, wakarudi haraka kutoka malishoni. Waliuia moyoni na kukasirika sana kwa saba-

33:17 *Maana yake “Mabanda; Vibanda.” 34:1 *Au “kuwaona.” 34:3 *Tnn., “kuzungumza na moyo wa msichana huyo.”

SURA YA 33

a Mwa 25:20
Mwa 28:6

b Yos 24:1

c Mwa 10:19
Mwa 12:6

d Yos 24:32
Mdo 7:15, 16

e Mwa 35:1, 7

SURA YA 34

f Mwa 30:19, 21
Mwa 46:15

g Mwa 26:34, 35
Mwa 27:46

h Kum 7:1
1Nya 1:13-15

i Mwa 33:18, 19

Safu ya 2

a 2Sa 13:22

b Ebr 13:4

c Mwa 24:2, 3

d Mwa 24:53
Ho 3:2

e Mwa 17:9, 12

f Mwa 17:10

bu Shekemu alikuwa amemfedhehesha Israeli kwa kumbaka binti ya Yakobo,^a jambo ambalo halipaswi kufanywa.^b

8 Hamori akazungumza nao, akisema: “Mwanangu Shekemu anamtamani sana* binti yenu. Tafadhali mpeni binti yenu awe mke wake, **9** na mfanye mapatano ya ndoa* pamoja nasi. Tupatieni mabinti wenu, nanyi mchukue mabinti wetu.^c **10** Mnaweza kuishi nasi na kukaa mahali popote nchini. Kaeni humu na kufanya biashara na kutulia nchini.” **11** Kisha Shekemu akamwambia baba ya Dina na ndugu zake: “Naomba nipate kibali machoni penu, nami nitawapa chochote mtakachoniomba. **12** Mnaweza kudai nitoe kiasi kikubwa sana cha mahari na zawadi.^d Niko tayari kuwapa chochote mtakachoniambia. Nipeni tu msichana huyu awe mke wangu.”

13 Wana wa Yakobo wakamjibu kwa hila Shekemu na Hamori baba yake, kwa sababu Shekemu alikuwa amembaka dada yao Dina. **14** Wakawaambia: “Hatuwezi kamwe kufanya jambo kama hilo, kukubali dada yetu aolewe na mwanamume ambaye hajatahiriwa,^e kufanya hivyo ni fedheha kwetu. **15** Tunaweza kukubali tu kwa sharti hili: watahirini wanaume wenu wote, muwe kama sisi.^f **16** Ndipo tutakapowapa mabinti wetu na kuwachukua mabinti wenu, nasi tutaishi nanyi na kuwa familia moja.

34:8 *Au “nafsi ya mwanangu Shekemu imeshikamana na.” 34:9 *Au “na muoane nasi.” 34:14 *Tnn., “aliye na govi.”

17 Lakini msipotusikiliza na kutahiriwa, basi tutamchukua binti yetu na kwenda zetu.”

18 Maneno yao yakamfurahisha Hamori^a na Shekemu mwanawe.^b **19** Kijana huyo hakukawia kutimiza ombi lao,^c kwa sababu alimpenda binti ya Yakobo, naye Shekemu aliheshimiwa kulioko watu wote wa nyumba ya baba yake.

20 Kwa hiyo Hamori na Shekemu mwanawe wakaenda kwenye lango la jiji, wakazungumza na wanaume wa jiji lao^d wakisema: **21** “Wanaume hawa wangependa tuishi nao kwa amani. Waruhusu ni wakae nchini na kufanya biashara humu, kwa maana nchi yetu ni kubwa vya kutosha. Tunaweza kuwaoa mabinti wao, nasi tunaweza kuwapa mabinti wetu.” **22** Lakini watakubali tu kuishi nasi ili tuwe familia moja kwa sharti hili moja: kwamba kila mwanamume miongoni mwetu atahiriwe kama tu wanavyotahiriwa.^f **23** Tukifanya hivyo, je, mali zao, utajiri wao, na mifugo yao yote haitakuwa yetu? Basi acheni tutimize sharti lao ili waishi nasi.” **24** Wote waliokuwa wakitoka nje kupitia lango la jiji lake wakamsikiliza Hamori na Shekemu mwanawe, na wanaume wote wakatahiriwa, wote waliokuwa wakitoka nje kupitia lango la jiji.

25 Hata hivyo, siku ya tatu, walipokuwa bado wana mau-mivu, wana wawili wa Yakobo, Simeoni na Lawi, ndugu za Dina,^g wakachukua kila mmoja wao upanga wake, wakaenda ghafla katika jiji hilo

SURA YA 34

a Mwa 33:18, 19

b Mwa 34:2

c Mwa 34:15

d Zek 8:16

e Mwa 34:8, 9

f Mwa 17:11

g Mwa 46:15

Safu ya 2

a Mwa 49:5-7

b Mwa 34:2

c Mwa 49:5

SURA YA 35

d Mwa 28:19
Mwa 31:13

e Mwa 27:42-44

f Mwa 31:19
Kum 5:7
Yos 23:7
1Ko 10:14

na kumuua kila mwanamume.^a **26** Wakamuua Hamori na Shekemu mwanawe kwa upanga, kisha wakamchukua Dina kutoka katika nyumba ya Shekemu na kuondoka. **27** Wana wengine wa Yakobo walipofika waliona maiti za wanaume waliouawa, wakalipora jiji hilo kwa sababu dada yao alibakwa.^b **28** Wakachukua kondoo wao, mbuti wao, ng'ombe wao, punda wao, na kitu chochote kilichokuwa jijini na shambani. **29** Walichukua pia mali zao zote, wakawachukua mateka wake zao na watoto wao wote, na kupora vitu vyote vilivyokuwa katika nyumba zao.

30 Basi Yakobo akawaambia Simeoni na Lawi:^c “Mmeniletea taabu kubwa* kwa kunifanya niwe uvundo kwa wakaaji wa nchi hii, Wakanaani na Waperizi. Nina watu wachache, nao kwa hakika wataungana na kunishambulia, nao wataniangamiza, mimi na nyumba yangu.” **31** Lakini wakamwambia: “Je, kuna yeye anayepaswa kumtendea dada yetu kama kahaba?”

35 Baada ya hayo Mungu akamwambia Yakobo: “Ondoka, nenda Betheli^d ukaiishi huko, na unijengee madhabu mimi Mungu wa kweli, niliyekutokea ulipokuwa ukimkimbia ndugu yako Esau.”^e

2 Basi Yakobo akawaambia watu wa nyumba yake na wote waliokuwa pamoja naye: “Ondoeni kabisa miungu ya kigeni iliyo kati yenu,^f na mjisafishe wenyewe na kubadili mavazi yenu, **3** na acheni tuondoke twende Betheli.

34:30 * Au “Mmenifanya nitengewe.”

Huko nitamjengea madhabahu Mungu wa kweli, aliyenijibu katika siku yangu ya taabu na ambaye amekuwa pamoja nami kila mahali nilipoenda.”^a **4** Basi wakampa Yakobo miungu yote ya kigeni walivyokuwa nayo na vipuli walivyovaa masikioni, kisha Yakobo akavifukia* chini ya mti mkubwa uliokuwa karibu na Shekemu.

5 Walipokuwa wakisafiri, hofu ya Mungu iliyakumba majiji yaliyowazunguka, kwa hiyo wakaaji wake hawakuwafuatia wana wa Yakobo. **6** Hatimaye Yakobo akafika Luzi,^b yaani, Betheli, katika nchi ya Kanaani, pamoja na watu wote waliokuwa naye. **7** Akajenga madhabahu huko na kupaita mahali hapo El-betheli,* kwa sababu Mungu wa kweli alikuwa ametokea mahali hapo alipomkimbia ndugu yake.^c **8** Baadaye Debora,^d mlezi wa Rebeke, akafa na kuzikwa chini ya mwaloni karibu na Betheli. Basi akaita mwaloni huo Alon-bakuthi.*

9 Mungu akamtokea Yakobo tena alipokuwa akitoka Padan-aramu, akambariki. **10** Mungu akamwambia: “Jina lako ni Yakobo.”^e Hutaitwa tena Yakobo, jina lako litakuwa Israeli.” Naye akaanza kumwita Israeli.^f **11** Mungu akaendelea kumwambia: “Mimi ni Mungu Mweza-Yote.^g Zaa uwe na watoto wengi. Mataifa na kusanyiko la mataifa litatoka kwako,^h na wafal-

35:3 *Au “katika njia niliyotembea.”
35:4 *Au “akavificha.” 35:7 *Maana yake “Mungu wa Betheli.” 35:8 *Maana yake “Mwaloni wa Kilio.”

SURA YA 35

a Mwa 28:13, 15
Mwa 31:42

b Mwa 28:19

c Mwa 28:20-22

d Mwa 24:59

e Mwa 25:26
Mwa 27:36

f Mwa 32:28

g Mwa 17:1
Kut 6:3
Ufu 15:3

h Mwa 48:3, 4

Safu ya 2

a Mwa 17:5, 6
Yoh 12:13

b Mwa 15:18
Kum 34:4

c Mwa 28:18

d Mwa 28:19

e Mwa 30:22-24

f Mwa 46:21
Mwa 49:27
Kum 33:12

g Mwa 48:7
Mik 5:2
Mt 2:6

me watatoka kwako.^a **12** Na nchi niliyompa Abrahamu na Isaka, nitakupua wewe na uzao wako* baada yako.”^b **13** Kisha Mungu akapanda na kumwacha mahali alipooongea naye.

14 Basi Yakobo akasimamisha nguzo mahali hapo alipooongea naye, nguzo ya mawe, naye akamimina toleo la kinywaji juu yake na pia akamimina mafuta juu yake.^c **15** Na Yakobo akaendelea kupaita mahali hapo ambapo Mungu alikuwa ameongea naye, Betheli.^d

16 Kisha wakaondoka Betheli. Na walipokuwa umbali fulani kabla ya kufika Efrathi, Raheli akaanza kuzaa, na uchungu wa kuzaa ulikuwa mkali sana. **17** Lakini alipokuwa aking’ang’ana kuzaa, mkunga akamwambia: “Usiogope, kwa maana utamzaa mwana huyu pia.”^e **18** Uhai wake ulipokuwa ukitoka (kwa kuwa alikuwa akifa), akamwita mwana huyo Ben-oni,* lakini baba yake akamwita Benjamin.^f **19** Kwa hiyo Raheli akafa na kuzikwa njiani kuelekea Efrathi, yaani, Bethlehemu.^g **20** Yakobo akasimamisha nguzo juu ya kaburi lake; hiyo ndiyo nguzo ya kaburi la Raheli mpaka leo hii.

21 Kisha Israeli akaendelea na safari na kupiga hema lake umbali fulani mbele ya mnara wa Ederi. **22** Siku moja, Israeli alipokuwa akiishi katika nchi hiyo, Rubeni alienda

35:11 *Tnn., “watatoka katika kiuno chako.” 35:12 *Tnn., “mbegu yako.” 35:18 *Maana yake “Mwana wa Maombolezo Yangu.” #Maana yake “Mwana wa Mkonu wa Kulia.”

na kulala na Bilha suria wa baba yake, naye Israeli akasiakia habari hizo.^a

Basi Yakobo alikuwa na wana 12. **23** Wana wa Lea walikuwa Rubeni,^b mzaliwa wa kwanza wa Yakobo, kisha Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, na Zabuloni. **24** Wana wa Raheli walikuwa Yosefu na Benjamini. **25** Na wana wa Bilha kijakazi wa Raheli walikuwa Dani na Naftali. **26** Na wana wa Zilpa kijakazi wa Lea walikuwa Gadi na Asheri. Hao ndio wana wa Yakobo waliozaliwa Padan-aramu.

27 Hatimaye Yakobo akafika mahali ambapo Isaka baba yake alikuwa kule Mamre,^c Kiriath-arba, yaani, Hebroni, ambako Abrahamu na pia Isaka waliishi wakiwa wageni.^d **28** Isaka aliishi miaka 180.^e **29** Kisha Isaka akakata pumzi na kufa, akazikwa pamoja na watu wake,* baada ya kuishi maisha marefu na yenye kuridhisha;^f na Esau na Yakobo wanawe wakamzika.^f

36 Hii ndiyo historia ya Esau, yaani, Edomu.^g

2 Esau alioa mabinti wa Kanaani: Ada^h binti ya Eloni Mhiti;ⁱ na Oholibama^j binti ya Ana, mjukuu wa Sibeoni Mhivi; **3** na Basemathi,^k binti ya Ishmaeli, dada ya Nebayothi.^l

4 Na Ada akamzalia Esau mtoto aliyetwa Elifazi, naye Basemathi akamzaa Reueli,

5 na Oholibama akamzaa Yeushi, Yalamu, na Kora.^m

Hao ndio wana wa Esau waliozaliwa katika nchi ya Ka-

35:29 *Tnn., "Akakusanywa kwa watu wake." Huu ni msemu wa kishairi unao-rejelea kifo. ^fTnn., "akiwa amezeeka na akiwa amejaa siku."

SURA YA 35

a Mwa 49:3, 4
1Nya 5:1

b Mwa 49:3

c Mwa 31:17, 18

d Mwa 15:13
Ebr 11:9

e Mwa 25:20, 26

f Mwa 49:30, 31

SURA YA 36

g Mwa 25:30
Eze 25:12, 13
Ro 9:13

h Mwa 36:10

i Mwa 26:34

j Mwa 36:18

k Mwa 36:17

l Mwa 25:13
Mwa 28:9

m 1Nya 1:35

Safu ya 2

a Mwa 33:9

b Mwa 27:39
Mwa 32:3

c Mwa 14:6
Kum 2:5

d Mwa 25:30

e Kum 2:12

f 1Nya 1:35

g Mwa 36:34

h Mwa 36:40, 42
1Nya 1:36

i Kut 17:8
Hes 13:29
Hes 24:20
Kum 25:19
1Sa 15:8
1Sa 30:1

j Mwa 26:34

naani. **6** Kisha Esau akawachukua wake zake, wanawe, mabinti zake, na watu wote wa nyumba yake, mifugo yake na wanyama wake wote, na mali yote aliyokusanya^a katika nchi ya Kanaani, akahamia nchi nyingine, umbali fulani kutoka kwa Yakobo ndugu yake.^b **7** Alihama kwa sababu mali zao zilikuwa nyingi sana wasiweze kuishi pamoja, na nchi walimoishi* haingewatosha kwa sababu walikuwa na mifugo mingi. **8** Kwa hiyo Esau akahamia eneo lenye milima la Seiri.^c Esau ndiye Edomu.^d

9 Na hii ndiyo historia ya Esau, baba ya Waedomu waliishi katika eneo lenye milima la Seiri.^e

10 Haya ndiyo majina ya wana wa Esau: Elifazi mwana wa Ada, mke wa Esau; Reueli mwana wa Basemathi, mke wa Esau.^f

11 Wana wa Elifazi walikuwa Temani,^g Omari, Sefo, Gatamu, na Kenasi.^h **12** Timna akawa suria wa Elifazi, mwana wa Esau. Baada ya muda akamzalia Elifazi mtoto aliyetwa Amaleki.ⁱ Hao ndio wana wa Ada, mke wa Esau.

13 Hawa ndio wana wa Reueli: Nahathi, Zera, Shamma, na Miza. Hao ndio waliokuwa wana wa Basemathi,^j mke wa Esau.

14 Hawa ndio waliokuwa wana wa Oholibama binti ya Ana, mjukuu wa Sibeoni, mke wa Esau, aliomzalia Esau: Yeushi, Yalamu, na Kora.

36:7 *Au "walimoishi wakiwa wageni."

15 Hawa ndio mashehe* wa wana wa Esau:^a Wana wa Elifazi, mzaliwa wa kwanza wa Esau: Shehe Temani, Shehe Omari, Shehe Sefo, Shehe Kenasi,^b **16** Shehe Kora, Shehe Gatamu, na Shehe Amaleki. Hao ndio mashehe wa Elifazi^c katika nchi ya Edomu. Hao ndio wana wa Ada.

17 Hawa ndio wana wa Reueli, mwana wa Esau: Shehe Nahathi, Shehe Zera, Shehe Shamma, na Shehe Miza. Hao ndio mashehe wa Reueli katika nchi ya Edomu.^d Hao ndio wana wa Basemathi, mke wa Esau.

18 Hatimaye hawa ndio wana wa Oholibama, mke wa Esau: Shehe Yeushi, Shehe Yalamu, na Shehe Kora. Hao ndio mashehe wa Oholibama binti ya Ana, mke wa Esau.

19 Hao ndio wana wa Esau, na hao ndio mashehe wao. Esau ndiye Edomu.^e

20 Hawa ndio wana wa Seiri, Mhori, wakaaji wa nchi:^f Lotani, Shobali, Sibeoni, Ana,^g **21** Dishoni, Ezeri, na Dishani.^h Hao ndio mashehe wa Wahori, wana wa Seiri, katika nchi ya Edomu.

22 Wana wa Lotani walikuwa Hori na Hemamu, naye dada ya Lotani alikuwa Timna.ⁱ

23 Hawa ndio wana wa Shobali: Alvani, Manahathi, Ebali, Shefo, na Onamu.

24 Hawa ndio wana wa Sibeoni:^j Aya na Ana. Huyu ndiye Ana aliyepata chemchemi za maji ya moto nyikani alipokuwa akiwachungua punda wa Sibeoni baba yake.

SURA YA 36

- a Kut 15:15
- b 1Nya 1:53, 54
- c 1Nya 1:36
- d Hes 20:23
1Fa 9:26
- e Mwa 25:30
Mwa 32:3
- f Mwa 14:6
Kum 2:12, 22
- g 1Nya 1:40
- h 1Nya 1:38
- i 1Nya 1:39
- j Mwa 36:2

Safu ya 2

- a 1Nya 1:41
- b 1Nya 1:42
- c 1Nya 1:38
- d Hes 20:14
- e Kum 17:14, 15
1Sa 10:19
1Nya 1:43-50
- f Mwa 25:1, 2
Kut 2:15
Hes 31:2

25 Hawa ndio watoto wa Ana: Dishoni na Oholibama binti ya Ana.

26 Hawa ndio wana wa Dishoni: Hemdani, Eshbani, Ithrani, na Kerani.^a

27 Hawa ndio wana wa Ezeri: Bilhani, Zaavani, na Akani.

28 Hawa ndio wana wa Dishani: Usi na Arani.^b

29 Hawa ndio mashehe wa Wahori: Shehe Lotani, Shehe Shobali, Shehe Sibeoni, Shehe Ana, **30** Shehe Dishoni, Shehe Ezeri, na Shehe Dishani.^c Hao ndio mashehe wa Wahori, kila shehe katika nchi ya Seiri.

31 Sasa hawa ndio wafalme waliotawala katika nchi ya Edomu^d kabla mfalme yeyote hajawatawala Waisraeli.^{*e} **32** Bela mwana wa Beori alitawala Edomu, na jiji lake liliitwa Dinhaba. **33** Bela alipokufa, Yobabu mwana wa Zera kutoka Bosra akaanza kutawala baada yake. **34** Yobabu alipokufa, Hushamu kutoka katika nchi ya Watemani akaanza kutawala baada yake.

35 Hushamu alipokufa, Hadadi mwana wa Bedadi aliyewashinda Wamidiani^f katika eneo* la Moabu akaanza kutawala baada yake, na jiji lake liliitwa Avithi. **36** Hadadi alipokufa, Samla kutoka Masreka akaanza kutawala baada yake. **37** Samla alipokufa, Shauli kutoka Rehobothi karibu na ule Mto akaanza kutawala baada yake. **38** Shauli alipokufa, Baal-hanani mwana wa Akbori akaanza kutawala baada yake. **39** Baal-hanani

36:31 *Tnn., "wana wa Israeli." **36:35** *Tnn., "shamba."

36:15 *Shehe alikuwa mkuu wa kabila.

mwana wa Akbori alipokufa, Hadari akaanza kutawala baada yake. Jiji lake liliitwa Pau, na mke wake alitwa Mehetabeli binti ya Matredi binti ya Mezahabu.

40 Basi haya ndiyo majina ya mashehe wa Esau kulingana na koo zao, kulingana na maeneo yao, kulingana na majina yao: Shehe Timna, Shehe Alva, Shehe Yethethi,^a **41** Shehe Oholibama, Shehe Ela, Shehe Pinoni, **42** Shehe Kenasi, Shehe Temani, Shehe Mibsari, **43** Shehe Magdieli, na Shehe Iramu. Hao ndio mashehe wa Edomu kulingana na sehemu walizoishi katika nchi waliyomiliki.^b Hao ndio wazao wa Esau, baba ya Waedomu.^c

37 Yakobo akaendelea kishi katika nchi ya Kanaani, alikoishi baba yake akiwa mgeni.^d

2 Hii ndiyo historia ya Yakobo.

Kijana Yosefu^e alipokuwa na umri wa miaka 17, alikuwa akichunga kondoo^f pamoja na wana wa Bilha^g na wana wa Zilpa,^h wake za baba yake. Naye Yosefu akamletea baba yake habari mbaya kuwahuu. **3** Sasa Israeli alimpenda sana Yosefu kuliko wanawe wengineⁱ kwa sababu alimzaa uzeeni, naye alikuwa amemshonea joho la pekee.* **4** Ndugu zake walipoona kwamba baba yao alimpenda sana kuliko yote miongoni mwao, wakaanza kumchukia, na hawakuzungumza naye kwa amani.

5 Baadaye Yosefu aliota ndoto na kuwasimulia ndugu zake,^j nao wakapata sababu zaidi ya kumchukia.

37:3 *Au "nguo ndefu maridadi."

SURA YA 36

a 1Nya 1:51-54

b Kum 2:5

c Mwa 25:30
Mwa 36:8

SURA YA 37

d Mwa 23:3, 4
Mwa 28:1, 4
Ebr 11:8, 9

e Mwa 30:25
Mwa 46:19

f Mwa 47:3

g Mwa 35:25

h Mwa 35:26

i 1Nya 2:1, 2

j Mwa 37:19

Safu ya 2

a Mwa 42:6, 9

b Mwa 45:8
Mwa 49:26

c Mwa 44:14
Mwa 45:9

d Mdo 7:9

e Mwa 33:18

f Mwa 23:19
Mwa 35:27

6 Aliwaambia hivi: "Tafadhali sikilizeni ndoto hii niliyoota. **7** Tulikuwa tukifunga matita ya masuke katikati ya shamba kisha tita langu likainuka na kusimama wima, nayo matita yenu yakalizinguka tita langu na kuliinamia."^a **8** Ndugu zake wakamuuliza: "Je, kweli utajiweka kuwa mfalme wetu na kututawala?"^b Basi wakapata sababu nyingine ya kumchukia, kwa sababu ya ndoto zake na mambo aliyosema.

9 Baada ya hayo akaota tena ndoto nyingine, naye akawasimulia ndugu zake ndoto hiyo: "Nimeota ndoto nyingine. Wakati huu jua na mwezi na nyota 11 zilikuwa zikiniinamia."^c **10** Kisha akamsimulia baba yake na ndugu zake ndoto hiyo, baba yake akamkemea na kumuuliza: "Ndoto hiyo yako inamaanisha nini? Je, kweli mimi na pia mama yako na ndugu zako tutakuja na kukuinamia mpaka ardhini?" **11** Basi ndugu zake wakazidi kumwonea wivu,^d lakini baba yake akaya-weka akilini maneno yake.

12 Sasa ndugu zake wakae-nda kulisha kondoo wa baba yao karibu na Shekemu.^e **13** Baadaye Israeli akamwambia Yosefu: "Ndugu zake wana- chunga kondoo karibu na Shekemu, sivyo? Njoo niku-tume kwao." Yosefu akamw-ambia: "Niko tayari!" **14** Ya-kobo akamwambia: "Tafadhali, nenda uone kama ndugu zako wako salama. Angalia hali ya kondoo, uniletee ha-bari." Basi akamtuma kuto-ka katika bonde la* Hebroni,^f

37:14 *Au "nchi tambarare ya chini ya."

naye akashika njia kuelekea Shekemu. **15** Baadaye mtu fulani akamkuta aki-tangatanga mbugani. Mtu huyo akamuuliza: “Unatafuta nini?” **16** Akamjibu: “Ninawatafuta ndugu zangu. Tafadhali niambie, wanachunga kondoo wapi?” **17** Mtu huyo akamwambia: “Wameondoka hapa, niliwasikia wakisema, ‘Twendeni Dothani.’” Kwa hiyo Yosefu akawafuata ndugu zake na kuwakuta Dothani.

18 Sasa wakamwona akiwa mbali, na kabla hajafika karibu, wakaanza kupanganjama ya kumuua. **19** Wakambiana: “Tazama! Ndiye yule mwota-ndoto anakuja.” **20** Haya basi, njooni tumuue na kumtupa ndani ya shimo moja la maji, halafu tutasema kwamba aliliwa na mnyama mkali sana wa mwituni. Tuone itakuwaje kwa ndoto zake.” **21** Rubeni^b aliposikia maneno hayo, alijaribu kumwokoia ili wasimuu. Akasema: “Tusimuu.”^c **22** Kisha akawaambia: “Msimwage damu.”^d Mtu-peni ndani ya shimo hili la maji lililo nyikani, lakini msimdhuru.”^e Rubeni alikusudia kumwokoia kutoka mikononi mwao ili amrudishe kwa baba yake.

23 Mara tu Yosefu alipowafikia ndugu zake, wakamvua joho lake la pekee,^f **24** kisha wakamchukua na kumtupa ndani ya shimo la maji. Wakati huo shimo hilo lilikuwa tupu; halikuwa na maji.

25 Kisha wakaketi chini ili wale chakula. Walipoinua macho yao, waliona msafara wa Waishmaeli^g ukija kuto-

SURA YA 37

a Mwa 37:5

b Mwa 49:3

c Mwa 9:5
Kut 20:13

d Mwa 4:8,10
Mwa 42:22

e Mwa 42:21

f Mwa 37:3

g Mwa 25:12

Safu ya 2

a Mwa 43:11

b Mwa 4:8,10

c Mdo 7:9

d Mwa 25:1, 2

e Mwa 40:15
Mwa 45:4
Zb 105:17

f Mwa 37:3

ka Gileadi. Ngamia wao walikuwa wamebeba gundi ya labdanamu, zeri, na magome yenye utomvu,^a nao walikuwa wakiteremka kwenda Misri. **26** Ndipo Yuda akawaambia ndugu zake: “Tutapata faida gani tukimua ndugu yetu na kufunika damu yake?”^b **27** Haya basi, acheni tumuuzec kwa Waishmaeli, mkono wetu usimguse. Kwa kweli, yeye ni ndugu yetu na nyama yetu.” Kwa hiyo wakamsikiliza ndugu yao. **28** Basi wafanyabiashara hao Wamidiani^d walipokuwa wakipita, ndugu zake walimtoa shimoni na kumuua kwa hao Waishmaeli kwa vipande 20 vya fedha.^e Watu hao wakampeleka Yosefu Misri.

29 Baadaye Rubeni aliporudi kwenye lile shimo la maji na kuona kwamba Yosefu hayumo shimoni, akayararua mavazi yake. **30** Aliporudi kwa ndugu zake, alisema kwa mshangao: “Mtoto amepotea! Sasa mimi—nitafanya nini?”

31 Basi wakalichukua joho la Yosefu, wakamchinja mbuzi dume na kulichovya joho hilo katika damu ya mbuzi huyo. **32** Kisha wakamtumia baba yao joho hilo na kumwambia: “Hiki ndicho tulichopata. Tafadhali chunguza uone ikiwa joho hili ni la mwanao au la.”^f

33 Basi akalichunguza na kusema kwa mshtuko: “Ni joho la mwanangu! Inaonekana ameliwa na mnyama mkali wa mwituni! Kwa hakika Yosefu ameraruliwa vipandevipande!”

34 Ndipo Yakobo akayararua mavazi yake na kuvaa nguo za magunia kiunoni na kumwombolezea mwanawe kwa siku nyingi. **35** Na wanawe wote

37:22 *Au “msimguse.”

na mabinti zake wote wakajaribu sana kumfariji, lakini alikataa kabisa kufarijiwa, akisema: “Nitashuka Kaburini*^a nikimwombolezea mwanangu!” Na baba yake akaendelea kumililia.

36 Basi Wamidiani wakaumuza Yosefu Misri kwa Potifa, ofisa wa makao ya Farao^b aliyekuwa pia mkuu wa walenzi.^c

38 Karibu wakati huo, Yuda aliwaacha ndugu zake na kupiga hema lake karibu na mwanamume Mwadulam aliyelitwa Hira. **2** Akiwa huko, Yuda akamwona binti ya Mkanaani fulani^d aliyelitwa Shua. Basi akamwoa na kulala naye, **3** akapata mimba. Baadaye akazaa mwana, akampa jina Eri.^e **4** Akapata mimba tena, akazaa mwana na kumpa jina Onani. **5** Kwa mara nyingine tena akazaa mwana na kumpa jina Shela. Shela alipozaliwa, Yuda alikuwa Akzibu.^f

6 Baada ya muda, Yuda akamtatua Eri mzaliwa wake wa kwanza mke aliyelitwa Tamari.^g **7** Lakini Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, alimchukiza Yehova; kwa hiyo Yehova akamuua. **8** Kwa hiyo, Yuda akamwambia Onani: “Lala na mke wa ndugu yako na ufunge naye ndoa ya ndugu mkwe, umpe ndugu yako mzao.”^h **9** Lakini Onani alijua kwamba mzao huyo hangehesabiwa kuwa wake.ⁱ Kwa hiyo alipolala na mke wa ndugu yake, alimwaga shahawa zake ardhini ili asimpe ndugu yake mzao.^j **10** Jambo ali-

37:35 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 37

a Mwa 42:38
Mwa 44:29
Zb 89:48
Mhu 9:10
Ho 13:14
Mdo 2:27
Ufu 20:13

b Mwa 39:1

c Mwa 40:2, 3

SURA YA 38

d Mwa 24:2, 3
Mwa 28:1

e Hes 26:19

f Yos 19:29, 31

g Mt 1:3

h Kum 25:5, 6
Mt 22:24

i Ru 4:6

j Kum 25:7, 9

Safu ya 2

a 1Nya 2:3

b Hes 26:19

c Mwa 38:2

d Yos 15:10, 12
Amu 14:1

e Mwa 38:1

f Kum 25:5

g Mwa 38:11

lofanya lilikuwa ovu machoni pa Yehova, kwa hiyo akamuua pia.^a **11** Yuda akamwambia Tamari binti mkwe wake: “Ishi ukiwa mjane katika nyumba ya baba yako mpaka Shela mwanangu atakapokua,” kwa maana Yuda alisema moyoni mwake: ‘Huenda yeye pia akafa kama ndugu zake.’^b Basi Tamari akaenda kuishi katika nyumba ya baba yake.

12 Muda fulani ukapita, na mke wa Yuda, aliyekuwa binti ya Shua,^c akafa. Yuda alizingatia kipindi cha maombolezo, kisha akaenda Timna^d kwa watumishi wake waliokata kondoo manyoya akiwa pamoja na rafiki yake, Hira, Mwadulam.^e **13** Tamari akaambiwa: “Baba mkwe wako anapanda kwenda Timna kuwakata kondoo wake manyoya.” **14** Ndipo akayavua mavazi yake ya ujane, akajifunika uso kwa shela na kujifunika mabegani kwa mtandio, akaketi chini kwenye lango la kuingia Enaimu, jiji lililo katika barabara inayokwenda Timna, kwa sababu aliona kwamba Shela amekuwa mtu mzima lakini hajaruhusiwa amwoe.^f

15 Yuda alipomwona, mara moja alifikiri yeye ni kahaba, kwa sababu alikuwa ameufunika uso wake. **16** Kwa hiyo, akamkaribia kando ya barabara na kumwambia: “Niruhusu tafadhali nilale nawe,” kwa maana hakujua kwamba alikuwa binti mkwe wake.^g Hata hivyo, Tamari akamuuliza: “Utanipa nini ili ulale nami?” **17** Akamjibu: “Nitakutumia mwanambuzi kutoka katika kundi langu.” Lakini akamuuliza: “Je, utanipa rehani kabla

hujamleta?” **18** Yuda akamuuliza: “Ungependa nikupe nini kama rehani?” akasema: “Pete yako ya muhuri^a na kamba yako na fimbo uliyoshika mkononi.” Basi akampa vitu hivyo na kulala naye, Tamari akapata mimba. **19** Baada ya hayo Tamari akainuka na kwenda zake, akavua mtandio aliojifunika na kuvaa mavazi yake ya ujane.

20 Basi Yuda akamtuma rafiki yake Mwadulamu^b ampelekee mwanamke huyo mwanambuzi ili amrudishie vitu alivyompa kama rehani, lakini hakumpata kamwe. **21** Akawauliza watu wa jiji hilo: “Yuko wapi yule kahaba wa hekaluni anayekaa kando ya barabara hapa Enaimu?” Lakini wakamjibu: “Hatujawahi kumwona kahaba yeyote wa hekaluni mahali hapa.” **22** Mwishowe akarudi kwa Yuda na kumwambia: “Sikumpata, na isitoshe watu wa jiji hilo waliniambia, ‘Hatujawahi kumwona kahaba yeyote wa hekaluni mahali hapa.’” **23** Basi Yuda akasema: “Mwache avichukue vitu hivyo, tusije tukadharauliwa. Usijali, nilikutuma umpelekee mwanambuzi huyu, lakini hukumpata.”

24 Hata hivyo, baada ya miezi mitatu hivi, Yuda aliambiwa: “Tamari binti mkwe wako amefanya ukahaba, na pia amepata mimba kwa sababu ya ukahaba wake.” Yuda akasema: “Mtoeni nje achemwe moto.”^c **25** Alipokuwa akitolewa nje, akatuma ujumbe huu kwa baba mkwe wake: “Mwenye vitu hivi ndiye aliyenipa mimba.” Kisha akasema: “Tafadhali chungu-

SURA YA 38

a Mwa 41:42
1Fa 21:8

b Mwa 38:1

c Law 21:9

Safu ya 2

a Mwa 38:16, 18

b Mwa 38:11
Kum 25:5

c Mwa 46:12
Ru 4:12
1Nya 2:4
Lu 3:23, 33

d Mt 1:3

SURA YA 39

e Zb 105:17
Mdo 7:9

f Mwa 37:36

g Mwa 17:20
Mwa 37:25

h Ro 8:31
Ebr 13:6

za vitu hivi ni vya nani, yaa-ni, pete hii ya muhuri na kamba na fimbo hii.”^a **26** Basi Yuda akavichunguza na kusema: “Yeye ni mwadilifu kuliko mimi, kwa sababu sikumruhusu Shela mwanangu amwoe.”^b Yuda hakufanya ngono naye tena baada ya hayo.

27 Wakati ulipofika wa Tamari kuzaa, mapacha walikuwa tumboni mwake. **28** Alipokuwa akizaa, mtoto mmoja alitoa mkono wake nje, na mara moja mkunga akachukua uzi mwekundu na kuu-funga mkono huo, akisema: “Huyu alitoka kwanza.” **29** Lakini mara tu alipouridisha mkono wake, ndugu yake akatoka, mkunga akasema kwa mshangao: “Lo! Umejipasulia njia!” Basi akapewa jina Perezī.^{*c} **30** Kisha ndugu yake aliyefungwa uzi mwekundu mkononi akatoka, akapewa jina Zera.^d

39 Basi Yosefu akapelekwa Misri,^e na Mmisri aliyeti-twa Potifa,^f ofisa wa makao ya Farao aliyekuwa pia mkuu wa walenzi, akamnunua kuto-ka kwa Waishmaeli^g waliomle-ta huko. **2** Lakini Yehova alikuwa pamoja na Yosefu.^h Kwa hiyo akafanikiwa na kuwekwa kuwa msimamizi wa nyumba ya bwana wake, yule Mmisri. **3** Bwana wake akaona kwamba Yehova alikuwa pamoja naye na kwamba Yehova alikuwa akifanikisha kila jambo alilokuwa akifanya.

4 Yosefu akaendelea kupata kibali machoni pa Potifa, naye akawa mhudumu wake binafsi. Kwa hiyo Potifa aka-

38:29 *Maana yake “Mpasuko,” labda li-narejelea hali ya kupasuka msamba.

mweka kuwa msimamizi wa nyumba yake, na wa vitu vyake vyote. **5** Tangu alipomweka kuwa msimamizi wa nyumba yake na wa vitu vyake vyote, Yehova aliendelea kubariki nyumba ya Mmisri huyo kwa sababu ya Yosefu, na Yehova akabariki vitu vyote alivyokuwa navyo nyumbani na shambani.^a **6** Hatimaye akamwachia Yosefu usimamizi wa vitu vyake vyote, naye hakujishughulisha na kitu chochote isipokuwa chakula chake. Isitoshe, Yosefu akawa mwanamume mwenye umbo zuri na sura inayopendeza.

7 Sasa baada ya hayo, mke wa bwana wake akaanza kumtupia jicho Yosefu na kumwambia: "Lala nami." **8** Lakini akakataa na kumwambia mke wa bwana wake: "Tazama, bwana wangu hajui vitu nilivyo navyo nyumbani, naye ameniweka kuwa msimamizi wa vitu vyake vyote. **9** Hakuna yeyote aliye mkuu zaidi yangu katika nyumba hii, naye hajanikataza kitu chochote isipokuwa wewe, kwa sababu wewe ni mke wake. Basi ninawezaje kufanya uovu huu mkubwa na kwa kweli nimtende Mungu dhambi?"^b

10 Basi siku baada ya siku alizungumza na Yosefu, lakini Yosefu hakukubali kamwe kulala naye wala kukaaka naye. **11** Lakini siku moja kati ya siku ambazo Yosefu aliingia nyumbani kufanya kazi yake, hakukuwa na mtumishi yeyote nyumbani. **12** Basi mke wa Potifa akaishika kwa nguvu nguo ya Yosefu akisema: "Lala nami!" Lakini Yosefu akaiacha nguo yake mikononi mwake na kukimbilia

SURA YA 39

a Mwa 30:27

b Mwa 2:24
Mwa 20:3, 6
Zb 51:Uta, 4
Mk 10:7, 8
Ebr 13:4

Safu ya 2

a Zb 105:17, 18

b Mwa 40:2, 3
Zb 105:19
Mdo 7:9

nje. **13** Mara tu mke wa Potifa alipoona kwamba Yosefu ameiacha nguo yake mikononi mwake na kukimbilia nje, **14** akaanza kulia kwa sauti kubwa na kuwaita wanaume wa nyumbani mwake na kuwaambia: "Tazameni! Alituletea mwanamume huyu Mwebrania ili tuwe kichekesho. Alikuwa kulala nami, lakini nikaanza kulia kwa sauti yangu vyote. **15** Mara tu aliposikia nikilia kwa sauti kubwa na kupiga mayowe, akaiacha nguo yake kando yangu na kukimbilia nje." **16** Kisha mke wa Potifa akaiweka nguo ya Yosefu kando yake mpaka bwana wake* aliporudi.

17 Halafu akamsimulia kisa hicho, akisema: "Yule mtumishi Mwebrania uliyetuletea alikuja kunifanya mimi niwe kichekesho. **18** Lakini mara tu nilipoanza kulia kwa sauti kubwa na kupiga mayowe, aliacha nguo yake kando yangu na kukimbilia nje." **19** Punde tu bwana wa Yosefu alipomsikia mke wake akisema: "Hayo ndiyo mambo ambayo mtumishi wako alinitendea," akawaka hasira. **20** Basi bwana wa Yosefu akamchukua Yosefu na kumtupa gerezeni, mahali ambapo wafungwa wa mfalme walifungwa, akabaki humo gerezeni.^a

21 Lakini Yehova aliendelea kuwa pamoja na Yosefu, naye akazidi kumtendea kwa upendo mshikamanifu na kumfanya apate kibali machoni pa ofisa mkuu wa gereza.^b

22 Kwa hiyo, ofisa mkuu wa gereza akamweka Yosefu

39:16 *Yaani, bwana wa Yosefu.

kuwa msimamizi wa wafu-
ngwa wote gerezani, na
wa kazi zote walizokuwa wa-
kifanya humo, yeye ndiye
aliyahakikisha zimefanywa.^a
23 Ofisa mkuu wa gereza ha-
kujishughulisha na jambo
hata moja lililokuwa chini
ya usimamizi wa Yosefu, kwa
maana Yehova alikuwa pamo-
ja na Yosefu na Yehova alifani-
kisha jambo lolote alilofanya.^b

40 Baada ya hayo, msima-
mizi mkuu wa vinywa-
ji^c na mwokaji mkuu wa mfalme
wa Misri walimkosea
bwana wao, mfalme wa Misri.
2 Kwa hiyo Farao akawakasi-
rikia vikali maafisa hao wa-
wili, msimamizi mkuu wa vi-
nywaji na mwokaji mkuu,^d
3 akawatupa katika gereza
lililokuwa katika nyumba
ya mkuu wa walenzi,^e mahali
ambapo Yosefu alikuwa ame-
fungwa.^f **4** Kisha mkuu wa
walenzi akamwagiza Yosefu
akae nao na kuwatumiza,^g nao
wakakaa gerezani kwa muda
fulani.*

5 Msimamizi wa vinywaji na
mwokaji wa mfalme wa Misri,
waliokuwa wamefungwa ge-
rezani, waliota ndoto usiku
mmoja, na kila ndoto ilikuwa
na maana yake.* **6** Asubuhi
iliyofuata, Yosefu alipoingia
na kuwaona, walionekana wa-
mehuzunika. **7** Basi akawau-
liza maafisa hao wa Farao wa-
liokuwa naye gerezani kati-
ka nyumba ya bwana wake:
“Mbona nyuso zenu zina
huzuni leo?” **8** Wakamjibu:
“Kila mmoja wetu aliota ndoto
lakini hakuna mtu wa kutuele-

40:4 *Tnn., “siku kadhaa.” 40:5 *Au
“fasiri yake.”

SURA YA 39
a Mwa 39:6

b Mwa 49:22, 25
Mdo 7:9, 10

SURA YA 40
c Mwa 40:11

d Mwa 40:20-22

e Mwa 37:36

f Mwa 39:20
Zb 105:17, 18

g Mwa 39:22

Safu ya 2

a Mwa 41:15, 16
Da 2:28, 45

b Mwa 41:12, 13

c Mwa 40:20, 21

d Mwa 37:28

e Mwa 39:7, 8

za maana yake.”* Yosefu aka-
waambia: “Je, si kazi ya Mu-
ngu kueleza maana ya ndoto?”^a
Tafadhali, nisimulieni ndoto
zenu.”

9 Basi msimamizi mkuu wa
vinywaji akamsimulia Yosefu
ndoto yake akisema: “Katika
ndoto yangu, niliona mzabibu
mbele yangu. **10** Na mzabi-
bu huo ulikuwa na matawi ma-
tatu, na ulipokuwa ukichipua
vitawi, ulichanua maua, na za-
bibu zilizokuwa kwenye visha-
da vyake zikaiva. **11** Na ki-
kombe cha Farao kilikuwa mi-
kononi mwangu, nami nika-
chukua zabibu na kukamua
ndani ya kikombe cha Farao.
Kisha nikakiweka kikombe
hicho mkononi mwa Fa-
rao.” **12** Ndiyo Yosefu aka-
mwambia: “Hii ndiyo maana
yake. Yale matawi matatu ni
siku tatu. **13** Siku tatu kuan-
zia leo, Farao atakutoa ge-
rezani* na kukurudisha kwe-
nye cheo chako,^b nawe utae-
ndelea kuweka kikombe cha
Farao mkononi mwake kama
ulivyokuwa ukifanya ulipo-
kuwa msimamizi wake wa vi-
nywaji.^c **14** Hata hivyo, uni-
kumbuke mambo yataka-
pokwenda vema. Tafadhali,
nitende kwa upendo mshika-
manifu na umwambie Farao
kunihusu, ili anitoe mahali
hapa. **15** Ukweli ni kwamba
nilitekwa nyara kutoka katika
nchi ya Waebrania,^d nami sija-
fanya kosa lolote linalostahili
nitupwe gerezani.”**e

16 Mwokaji mkuu alipoo-
na kwamba Yosefu amese-
ma* jambo jema kuhusu ndo-

40:8 *Au “hatuna mfasiri.” 40:13
*Tnn., “atakiinua juu kichwa chako.”
40:15 *Tnn., “ndani ya tangi la maji; shi-
moni.” 40:16 *Au “amefasiri.”

to hiyo, akamwambia: “Mimi pia niliota ndoto, kulikuwa na vikapu vitatu vyenye mikate myeupe juu ya kichwa changu, **17** na katika kikapu cha juu, kulikuwa na kila aina ya vitu vilivyookwa kwa ajili ya Farao, na kulikuwa na ndege waliokula vitu vilivyokuwa katika kikapu kilichokuwa juu ya kichwa changu.” **18** Ndipo Yosefu akamwambia, “Hii ndiyo maana yake: Vile vikapu vitatu ni siku tatu. **19** Siku tatu kuanzia leo, Farao atakukata kichwa na kukutundika mtini, na ndege wataula mwili wako.”^a

20 Sasa siku ya tatu ilikuwa sikukuu ya kuzaliwa kwa Farao,^b kwa hiyo aliwafanyia karamu watumishi wake wote, akamtoa gerezani msimamizi mkuu wa vinywaji na mwokaji mkuu, akawaleta mbele ya watumishi wake. **21** Akamrudisha msimamizi mkuu wa vinywaji kwenye cheo chake, akaendelea kumpa Farao kikombe. **22** Lakini akamtundika mwokaji mkuu, kama Yosefu alivyokuwa ameeleza.*^c **23** Hata hivyo, msimamizi mkuu wa vinywaji hakumkumbuka Yosefu; aliendelea kumsahau.^d

41 Mwishoni mwa miaka miwili kamili, Farao aliota ndoto;^e katika ndoto hiyo alikuwa amesimama kando ya Mto Nile. **2** Na tazama! ng’ombe saba wazuri, walionona, walikuwa wakipanda kutoka mtoni, nao walikuwa wakila nyasi za Mto Nile.^f **3** Baada yao, ng’ombe wengine saba wenye sura mbaya na waliokonda walipanda kutoka

SURA YA 40

a Mwa 40:20, 22

b Mk 6:21

c Mwa 40:8

d Mwa 40:14

SURA YA 41

e Da 2:1

f Mwa 41:18-21

Safu ya 2

a Mwa 41:22-24

b Mwa 40:2, 3

c Mwa 40:5

katika Mto Nile, wakasimama karibu na wale ng’ombe wanonono kwenye ukingo wa Mto Nile. **4** Kisha wale ng’ombe wenye sura mbaya, waliokonda, wakaanza kuwala wale ng’ombe saba wazuri, walionona. Ndipo Farao akaamka.

5 Kisha akarudi kulala, akaota ndoto ya pili. Kulikuwa na masuke saba ya nafaka yakitokea katika bua moja, yalikuwa yamejaa nafaka nayo yalikuwa mazuri sana.^a **6** Na baada ya hayo, masuke mengine saba ya nafaka yakakua, yalikuwa membamba na yalikuwa yamechomwa na upepo wa mashariki. **7** Kisha masuke hayo membamba ya nafaka yakaanza kuyameza yale masuke saba ya nafaka yaliyojaa nafaka na ambayo yalikuwa mazuri sana. Ndipo Farao akaamka na kugundua kwamba ilikuwa ndoto.

8 Lakini asubuhi, roho yake ikafadhaika. Basi akaagiza makuhani wote wachawi wa Misri na watu wake wote wenye hekima waitwe. Farao akawasimulia ndoto zake, lakini hakuna yeyote aliyeweza kumwambia Farao maana yake.*

9 Ndipo msimamizi mkuu wa vinywaji akamwambia Farao: “Ninaungama dhambi zangu leo. **10** Ee Farao, ulitukasirikia sisi watumishi wako. Kwa hiyo ukanifunga gerezani katika nyumba ya mkuu wa walenzi, mimi na mwokaji mkuu.^b **11** Kisha kila mmoja wetu akaota ndoto usiku uleule. Yeye na mimi, kila mmoja wetu aliota ndoto, na kila ndoto ilikuwa na maana yake.^c

41:8 *Au “fasiri yake.”

40:22 *Au “amefasiri.”

12 Humo gerezani tulikuwa pamoja na kijana Mwebrania, mtumishi wa mkuu wa wali-nzi.^a Tulipomsimulia ndoto zetu,^b alitueleza maana ya kila ndoto. **13** Mambo yote yalitimia kama alivyotuambia.* Nilirudishwa katika cheo changu, lakini yule mwingine alitundikwa mtini.”^c

14 Kwa hiyo Farao akaagiza Yosefu aletwe,^d basi wakamleta haraka kutoka gerezani.*^e Akajinyoa na kubadili nguo zake na kuingia mbele ya Farao. **15** Kisha Farao akamwambia Yosefu: “Niliota ndoto, lakini hakuna yeyote anayeweza kunieleza maana yake. Sasa nimesikia habari zako kwamba ukisimuliwa ndoto unaweza kueleza maana yake.”^f **16** Ndipo Yosefu akamjibu Farao: “Sistahili kusifiwa! Mungu ndiye atakayesema kuhusu hali yako, Ee Farao.”^g

17 Farao akamwambia Yosefu: “Katika ndoto yangu, nilikuwa nimesimama kwenye ukingo wa Mto Nile. **18** Na tazama! ng’ombe saba wazuri, walionona, walikuwa wakipanda kutoka katika Mto Nile, wakaanza kula nyasi za Mto Nile.^h **19** Baada yao, ng’ombe wengine saba dhaidu, wenye sura mbaya sana, na waliokonda walipanda kutoka katika Mto Nile. Sijawahi kamwe kuona ng’ombe wenye sura mbaya hivyo katika nchi yote ya Misri. **20** Na ng’ombe hao waliokonda, wenye sura mbaya, wakaanza kuwala wale ng’ombe saba wa kwanza walionona. **21** Lakini baada ya kuwala, hakuna

41:13 *Au “alivyotufasiria.” 41:14 *Tnn., “ndani ya tangi la maji; shimoni.”

SURA YA 41

a Mwa 39:1

b Mwa 40:8

c Mwa 40:21, 22

d Zb 105:20

e Mwa 40:15

f Da 5:12
Mdo 7:9, 10

g Mwa 40:8
Da 2:23, 28

h Mwa 41:2-4

Safu ya 2
a Mwa 41:5-7

b Mwa 41:8
Da 2:2

c Da 2:27
Da 4:7

d Da 2:28
Amo 3:7

yeyote ambaye angejua kwa-mba wamewala ng’ombe hao, kwa kuwa sura yao ilikuwa mbaya kama mwanzoni. Ndipo nikaamka.

22 “Kisha nikaona katika ndoto yangu masuke saba ya nafaka yakitokea katika bua moja, yalikuwa yamejaa nafaka nayo yalikuwa mazuri sana.^a **23** Halafu yakafuatwa na masuke engine saba ya nafaka yaliyonyauka, membamba, na yaliyochomwa na upepo wa mashariki. **24** Kisha yale masuke membamba ya nafaka yakaanza kuyameza yale masuke saba mazuri sana ya nafaka. Basi nikawasimulia makuhani wachawi ndoto hiyo,^b lakini hakuna yeyote aliyeweza kunieleza maana yake.”^c

25 Ndipo Yosefu akamwambia Farao: “Ndoto zako ni ndoto moja, ndoto ileile. Mungu wa kweli amekwambia mambo atakayofanya.”^d

26 Wale ng’ombe saba wazuri ni miaka saba. Na yale masuke saba mazuri ya nafaka ni miaka saba pia. Ndoto zako ni ndoto moja, ndoto ileile. **27** Wale ng’ombe saba waliokonda na wenye sura mbaya ambao walipanda baada ya wale wanono, ni miaka saba, na yale masuke saba ya nafaka yaliyo matupu, yaliyochomwa na upepo wa mashariki, yanamaanisha miaka saba ya njaa kali. **28** Hivi ndivyo nilivyokuambia, Ee Farao: Mungu wa kweli amekuonyesha mambo atakayofanya.

29 “Kutakuwa na miaka saba ya chakula kingi sana katika nchi yote ya Misri. **30** Lakini baada ya miaka hiyo, hakika kutakuwa na mia-

ka saba ya njaa kali, nanyi hakika mtasahau chakula kingi sana kilichokuwa katika nchi ya Misri, na njaa hiyo kali itaiharibu nchi.^a **31** Nanyi hamtakumbuka chakula kingi sana kilichokuwa nchini kwa sababu ya njaa kali itakayofuata, kwa maana itakuwa kali sana. **32** Ee Farao, ulionyesha ndoto hiyo mara mbili kwa sababu Mungu wa kweli amekusudia kabisa jambo hilo, na Mungu wa kweli atalitimizea hivi karibuni.

33 "Sasa basi, Ee Farao, mtafute mwanamume mwenye busara na hekima umweke kuwa msimamizi wa nchi ya Misri. **34** Ee Farao, chukua hatua, waweke wasimamizi nchini, nawe utakusanya sehemu ya tano ya mazao yote nchini Misri katika miaka saba ya chakula kingi.^b **35** Nao wakusanye chakula chote katika miaka hiyo mizuri inayokuja, nao waweke nafaka katika maghala chini ya mamlaka yako Farao, na chakula hicho kihifadhiwe na kutunzwa katika majiji.^c **36** Chakula hicho kitaliwa nchini katika ile miaka saba ya njaa kali itakayoikumba nchi ya Misri, ili nchi isiingamie kwa sababu ya njaa hiyo kali."^d

37 Pendekezo hilo lilimfurahisha Farao na watumishi wake wote. **38** Kwa hiyo Farao akawaambia watumishi wake: "Je, kweli kuna mwanamume mwingine anayeweza kupatikana kama huyu aliye na roho ya Mungu?" **39** Kisha Farao akamwambia Yosefu: "Kwa kuwa Mungu amekuwezesha kuyajua yote hayo,

SURA YA 41

a Mdo 7:11

b Mwa 41:26, 47

c Mwa 41:48, 49
Mdo 7:12d Mwa 45:9, 11
Mwa 47:13, 19

Safu ya 2

a Mwa 39:6
Zb 105:21
Mdo 7:9, 10

b Da 5:7

c Mwa 44:18
Mwa 45:8
Mdo 7:9, 10

d Mwa 46:20

e Zb 105:21

f Hes 4:3
2Sa 5:4
Lu 3:23

hakuna yeyote aliye na busara na hekima kama wewe.

40 Wewe binafsi utaisimamia nyumba yangu, na watu wangu wote watakutii kabisa.^a Nitakuwa tu mkuu kuliko wewe ninapotimiza jukumu langu nikiwa mfalme."^b

41 Kisha Farao akamwambia Yosefu: "Tazama, ninakuweka kuwa msimamizi wa nchi yote ya Misri."^b **42** Halafu Farao akaivua pete yake ya muhuri kutoka kwenye mkono wake mwenyewe na kumvisha Yosefu mkononi, akamvisha pia mavazi ya kitani bora na mkufu wa dhahabu shingoni mwake. **43** Zaidi ya hayo, akampandisha katika gari lake la pili la heshima, na watu walikuwa wakimtangulia na kusema kwa sauti, "Avrekh!"^c Kwa hiyo Farao akamweka kuwa msimamizi wa nchi yote ya Misri.

44 Tena Farao akamwambia Yosefu: "Mimi ni Farao, lakini hakuna mtu anayepaswa kufanya jambo lolote* bila idhini yako katika nchi yote ya Misri."^c **45** Kisha Farao akampa Yosefu jina Zafenath-panea, na pia akampa Asenathi^d binti ya Potifera kuhani wa Oni* awe mke wake. Naye Yosefu akaanza kuisimamia^e nchi ya Misri.^e **46** Yosefu alikuwa na umri wa miaka 30^f alipoanza kumtumikia* Farao mfalme wa Misri.

41:40 *Au "inapohusu tu kiti cha ufalme." **41:43** *Inaonekana ni neno linalowaamuru watu waonyeshe heshima na staha. **41:44** *Tnn., "kuinua mkono wake au mguu wake." **41:45** *Yaan, Heliopolisi. ^aAu "kutembea kotekote katika." **41:46** *Tnn., "aliposimama mbele ya."

Kisha Yosefu akaondoka mbele ya Farao na kute-mbea katika nchi yote ya Misri. **47** Na katika miaka saba ya chakula kingi, nchi ilizaa chakula kingi sana. **48** Naye aliendelea kukusanya chakula chote cha miaka saba katika nchi ya Misri, akakiweka katika maghala majijini. Katika kila jiji alikusanya chakula kutoka katika mashamba yaliyozunguka jiji hilo. **49** Yosefu akaendelea kukusanya nafaka nyingi sana katika maghala, kama mchanga wa bahari, hivi kwamba mwishowe wakaacha kuipima kwa sababu haingeweza kupimwa.

50 Kabla ya mwaka wa kwanza wa njaa kali, Asenathi, binti ya Potifera kuhani wa Oni* alimzalia Yosefu wana wawili.^a **51** Yosefu alimwita mzaliwa wa kwanza Manase,^{*b} kwa maana alisema, “Mungu amenifanya nisahau taabu yangu yote na nyumba yote ya baba yangu.” **52** Akamwita yule wa pili Efraimu,^{*c} kwa maana alisema, “Mungu ameniwezesha kuzaa watoto katika nchi ya mateso yangu.”^d

53 Hatimaye miaka saba ya chakula kingi katika nchi ya Misri ikaisha,^e **54** na miaka saba ya njaa kali ikaanza, kama Yosefu alivyokuwa amesema.^f Njaa hiyo ilienea katika nchi zote, lakini kulikuwa na chakula* katika nchi yote ya Misri.^g **55** Mwishowe, nchi yote ya Misri ikakumbwa na njaa hiyo kali, watu wakaanza kumlilia Farao awape chaku-

41:50 *Au “Heliopolisi.” 41:51 *Maana yake “Anayesahaulisha; Anayemfanya Mwingine Asahau.” 41:52 *Maana yake “Anayezaa Maradufu.” 41:54, 55 *Au “mkate.”

SURA YA 41

- a Mwa 48:5
- b Mwa 50:23
Hes 1:34, 35
- c Mwa 48:17
Hes 1:32, 33
Kum 33:17
Yos 14:4
- d Zb 105:17, 18
Mdo 7:9, 10
- e Mwa 41:26
- f Mwa 41:30
Mdo 7:11
- g Mwa 45:9, 11
Mwa 47:17

Safu ya 2

- a Mwa 47:13
- b Zb 105:21
- c Mwa 43:1
- d Mwa 41:48, 49
Mwa 47:16
- e Mwa 47:4

SURA YA 42

- f Mwa 41:48, 49
- g Mdo 7:12
- h 1Nya 2:1, 2
- i Mwa 35:18, 19
Mwa 42:38
Mwa 44:20
- j Mwa 43:14
- k Mwa 41:57
Mdo 7:11
- l Mwa 41:44
Mwa 45:8
Zb 105:21
Mdo 7:9, 10
- m Mwa 47:14
- n Mwa 37:7, 9
- o Mwa 42:23

la.^{*a} Basi Farao akawaambia Wamisri wote: “Nendeni kwa Yosefu, na mfanye lolote atakalowaambia.”^b **56** Njaa hiyo ikaenea duniani pote.^c Ndi-po Yosefu akaanza kuyafungua maghala yote ya nafaka yaliyokuwa katika majiji yao na kuwauzia Wamisri chakula,^d kwani njaa hiyo ilikuwa imeilemea sana nchi ya Misri. **57** Isitoshe, watu kutoka kila mahali duniani wakaja Misri kununua chakula kutoka kwa Yosefu, kwa sababu njaa hiyo ilikuwa imeilemea sana dunia yote.^e

42 Yakobo aliposikia kwamba kuna nafaka nchini Misri,^f akawauliza wanawe: “Kwa nini mnatazamana tu?” **2** Kisha akawaambia: “Nimesikia kwamba kuna nafaka nchini Misri. Shukeni huko mkatununulie nafaka, ili tundelee kuishi tusije tukafa.”^g **3** Basi ndugu kumi wa Yosefu^h wakashuka Misri kununua nafaka. **4** Lakini Yakobo hakumruhusu Benjamini,ⁱ ndugu ya Yosefu, aende pamoja na ndugu zake, kwa sababu alisema: “Huenda akapatwa na madhara na kufa.”^j

5 Kwa hiyo wana wa Israeli wakafika Misri pamoja na watu wengine walioenda kununua nafaka, kwa sababu njaa hiyo kali ilikuwa imeenea mpaka katika nchi ya Kanaani.^k **6** Yosefu ndiye aliyekuwa msimamizi nchini Misri,^l na ndiye aliyewauzia nafaka watu wote duniani.^m Kwa hiyo ndugu za Yosefu wakaja na kumwinamia kifudifudi.ⁿ **7** Yosefu alipowabona ndugu zake, aliwatambua mara moja, lakini haku-jitambulisha kwao.^o Basi aka-

wauliza kwa ukali: “Mmetoka wapi?” wakamjibu: “Katika nchi ya Kanaani, tumekuja kununua chakula.”^a

8 Basi Yosefu akawatambua ndugu zake, lakini wao hawakumtambua. **9** Mara moja Yosefu akakumbuka ndoto alizoota kuwahusu,^b akawaambia: “Ninyi ni wapelelezi! Mmekuja kuchunguza udhaifu wa nchi yetu!” **10** Wakawambia: “Hapana, bwana wetu, sisi watumishi wako tumekuja kununua chakula. **11** Sisi sote ni wana wa mtu mmoja. Nasi ni wanyoofu. Sisi watumishi wako si wapelelezi.” **12** Lakini akawaambia: “Sivyo! Mmekuja kuchunguza udhaifu wa nchi yetu!” **13** Ndipo wakawambia: “Sisi watumishi wako, ni ndugu 12.^c Sisi ni wana wa mtu mmoja^d anayeishi nchini Kanaani, na ndugu yetu mdogo amebaki na baba yetu,^e lakini mwingine hayupo tena.”^f

14 Hata hivyo, Yosefu akawaambia: “Ni kama tu nilivyowaambia—‘Ninyi ni wapelelezi!’ **15** Hivi ndivyo mtakavyojaribiwa: Kwa hakika kama Farao anavyoishi, hamtatokea mahali hapa mpaka ndugu yetu mdogo atakapokuja.”^g **16** Mtumeni mmoja wenu akamlete ndugu yenu, lakini ninyi wengine mtatiwa kifungoni. Kwa njia hiyo, maneno yenu yatajaribiwa ili ijulikane ikiwa mnasema ukweli. Na kama siuyo, basi, kwa hakika kama Farao anavyoishi, ninyi ni wapelelezi.” **17** Ndipo akawatia kifungoni kwa siku tatu.

18 Siku ya tatu, Yosefu akawaambia: “Fanyeni hili ili mwendelee kuishi, kwa sababu ninamwogopa Mungu.

SURA YA 42

a Mwa 37:1
Mdo 7:11,12

b Mwa 37:7-9

c 1Nya 2:1,2

d Kut 1:1-4

e Mwa 35:18,19
Mwa 42:38
Mwa 43:7

f Mwa 37:27,35
Mwa 44:20

g Mwa 42:34
Mwa 43:29

Safu ya 2

a Mwa 45:21,23

b Mwa 37:18,28
Mwa 50:17
Mdo 7:9

c Mwa 37:21

d Mwa 9:5

e Mwa 43:30

f Mwa 42:19

g Mwa 43:23

19 Ikiwa ninyi ni wanyoofu, acheni ndugu yenu mmoja abaki katika nyumba ambamo mmefungiwa, lakini ninyi wengine mnaweza kwenda kuchukua nafaka ili mpunguze makali ya njaa katika nyumba zenu.^a **20** Kisha mleteni kwangu ndugu yenu mdogo, ili maneno yenu yathibitike kuwa ya kweli, nanyi hamtakufa.” Basi wakafanya hivyo.

21 Wakaambiana: “Bila shaka tunaadhibiwa kwa sababu ya ndugu yetu,^b kwa sababu tuliyaona mateso yake alipotusihitumhurumie, lakini hatukumsikiliza. Ndiyo sababu tunateseka hivi.” **22** Kisha Rubeni akawaambia: “Je, sikuwaambia, ‘Msimdhuru mtoto,’^{*} lakini hamkunisikiliza?^c Sasa kwa hakika tuna daiwa damu yake.”^d **23** Lakini hawakujua kwamba Yosefu alielewa mambo waliyokuwa wakisema, kwa sababu aliongea nao kupitia mkalimani. **24** Basi akaenda mbali nao na kuanza kulia.^e Aliporudi na kuzungumza nao, alimchukua Simeoni^f kutoka kati yao na kumfunga mbele ya macho yao.^g **25** Kisha Yosefu akaamuru mifuko yao ijazwe nafaka, na pesa za kila mmoja wao zirudishwe ndani ya gunia lake na pia wapewe vyakula kwa ajili ya safari. Ndivyo walivyofanyiwa.

26 Basi wakawatwika punda wao nafaka na kuondoka. **27** Walipofika mahali pa kulala, mmoja wao alifungua gunia lake ili amlishe punda wake, akaona pesa kwenye mdomo wa mfuko wake.

42:22 * Tnn., “Msitende dhambi dhidi ya mtoto huyu.”

28 Akawaambia ndugu zake: “Pesa zangu zimerudishwa, ndizo hizi hapa kwenye mfuko wangu!” Wakashuka moyo, wakaanza kutetemeka na kuulizana: “Ni jambo gani hili ambalo Mungu ametutendea?”

29 Walipofika kwa Yakobo baba yao katika nchi ya Kanaani, wakamwambia mambo yote yaliyowapata, wakisema:

30 “Bwana mkubwa wa nchi hiyo alizungumza nasi kwa ukali^a na kudai kwamba tunaipeleleza nchi yao. **31** Lakini tukamwambia, ‘Sisi ni watu wanyoofu. Sisi si wapelelezi.’^b

32 Sisi ni ndugu 12,^c wana wa baba mmoja. Mmoja wetu hayupo,^d na yule mdogo amebaki na baba yetu katika nchi ya Kanaani.’^e **33** Lakini bwana huyo akatuambia, ‘Hivi ndivyo nitakavyoomba kwamba ninyi ni wanyoofu: Kwacheni ndugu yenu mmoja abaki nami.’^f Kisha chukueni chakula mwende mkapunguze makali ya njaa ya watu wa nyumbani mwenu.’^g **34** Mleteni kwangu ndugu yenu mdogo, ili nijue kwamba ninyi si wapelelezi bali ni watu wanyoofu. Kisha nitamrudisha ndugu yenu, nanyi mnaweza kufanya biashara katika nchi hii.”

35 Walipokuwa wakimwaga nafaka kutoka katika magunia yao, kila mmoja wao alipata mfuko wake wa pesa katika gunia lake. Wote pamoja na baba yao walipoona mfuko yao ya pesa, wakaogopa. **36** Yakobo baba yao akashtuka na kusema: “Mmefanya nifiwe!^h Yosefu hayupo,ⁱ Si-meoni naye hayupo,^j na sasa mnataka kumchukua Benjamin! Mambo hayo yote yame-nijia mimi!” **37** Lakini Rube-

SURA YA 42

- a Mwa 42:7, 9
- b Mwa 42:11
- c Mwa 42:13
- d Mwa 37:28, 35
- e Mwa 35:18, 19
Mwa 42:4
- f Mwa 42:19
- g Mwa 42:2
- h Mwa 43:14
- i Mwa 37:28, 35
- j Mwa 42:24

Safu ya 2

- a Mwa 37:22
Mwa 46:9
- b Mwa 43:8, 9
Mwa 44:32
- c Mwa 37:31-34
Mwa 44:20
- d Zb 89:48
Mhu 9:10
Ho 13:14
Mdo 2:27
Ufu 20:13
- e Mwa 37:34, 35
Mwa 44:29

SURA YA 43

- f Mwa 41:30
Mdo 7:11
- g Mwa 42:1, 2
- h Mwa 42:15
- i Mwa 42:15
- j Mwa 32:28
- k Mwa 42:13
- l Mwa 42:16

ni akamwambia baba yake: “Unaweza kuwaua wanangu wawili nisipomrudisha kwako.^a Mweke chini ya uangalizi wangu, nami nitamrudisha kwako.”^b **38** Lakini Yakobo akasema: “Mwanangu hatashuka huko pamoja nanyi, kwa sababu ndugu yake amekufa, naye amebaki peke yake.^c Akipatwa na madhara na kufia njiani, basi kwa hakika mtazishusha mvi zangu Kaburini*^d kwa huzuni.”^e

43 Sasa njaa ilikuwa kali sana nchini.^f **2** Basi walipomaliza kula nafaka waliyoleta kutoka Misri,^g baba yao akawaambia: “Rudini huko mkatununulie chakula kidogo.” **3** Yuda akamwambia: “Yule mtu alituonya waziwazi akisema, ‘Msiuone tena uso wangu msipokuja na ndugu yenu.’^h **4** Ukituruhusu twende na ndugu yetu, tutashuka huko na kukununulia chakula. **5** Lakini usipoturuhusu twende naye, hatutashuka kwenda huko, kwa sababu mtu huyo alituambia, ‘Msiuone uso wangu tena msipokuja na ndugu yenu.’”ⁱ

6 Israeli^j akawauliza: “Kwa nini mmeniletea shida hii kwa kumwambia mtu huyo kwamba mna ndugu mwingine?” **7** Wakamjibu: “Mtu huyo alituuiliza hivi moja kwa moja kutuhusu sisi na watu wetu wa ukoo: ‘Je, baba yenu angali hai? Je, mna ndugu mwingine?’ nasi tukamwambia ukweli.^k Tungejua je atasema, ‘Mleteni ndugu yenu huku chini?’”^l

8 Kisha Yuda akamsihi Israeli baba yake: “Niruhusu

42:38 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

niende na mvulana huyu,^a acha twende zetu ili tuishi tu-sije tukafa^b—wewe na sisi na watoto wetu.^c **9** Nitaku-wa dhamana kwa ajili ya uli-nzi wake.^{*d} Nitawajibika kwa-ko. Nisipomrudisha na kuku-kabidhi, nitakuwa nimekute-ndea dhambi ya kudumu. **10** Lakini ikiwa hatungalika-wia, kufikia sasa tungalikuwa tumefika huko na kurudi mara mbili.”

11 Kwa hiyo Israeli baba yao akawaambia: “Ikiwa ni lazima iwe hivyo, basi fa-nyeni hivi: Bebeni katika mi-fuko yenu vitu bora zaidi vya nchi yetu mkampelekee mtu huyo zawadi:^e zeri^f kidogo, asali kidogo, labdanamu, magome yenye utomvu,^g kungu, na lozi. **12** Bebeni kiasi maradufu cha pesa; na pia rudisheni pesa zilizowe-kwa kwenye midomo ya mi-fuko yenu.^h Huenda walikosea. **13** Mchukueni ndugu yenu mwende, rudini kwa mtu huyo. **14** Mungu Mweza-Yote na amchoche mtu huyo awa-hurumie, ili awaruhusu mrudi na yule ndugu yenu mwingine na Benjamini. Lakini ikiwa ni lazima nifiwe, basi nitafiwa!”ⁱ

15 Kwa hiyo wanaume hao wakachukua zawadi hiyo, kiasi maradufu cha pesa, na pia wakamchukua Benjamini. Wa-kaondoka na kushuka Misri, wakafika na kusimama tena mbele ya Yosefu.^j **16** Yosefu alipomwona Benjamini aki-wa pamoja nao, mara moja akamwambia msimamizi wa nyumba yake: “Wapeleke watu hawa nyumbani, uchinje wa-nyama na kutayarisha cha-

SURA YA 43

a Mwa 37:26
Mwa 42:38

b Mwa 42:1, 2

c Mdo 7:14

d Mwa 44:32

e Mwa 32:20

f Yer 8:22
Eze 27:17

g Mwa 37:25

h Mwa 42:25, 35

i Mwa 42:36

j Mwa 37:7, 9

Safu ya 2

a Mwa 41:39, 40

b Mwa 42:25, 35

c Mwa 42:3

d Mwa 42:27

e Mwa 43:12

f Mwa 42:23, 24

g Mwa 43:11

kula, kwa sababu watakula nami chakula cha mchana.” **17** Mara moja mtu huyo akafanya kama Yosefu alivyo-mwambia,^a akawapeleka nyumbani kwa Yosefu. **18** Lakini waliogopa walipopele-kwa nyumbani kwa Yosefu, wakaanza kusema: “Tumele-twa hapa kwa sababu ya zile pesa zilizorudishwa katika mi-fuko yetu wakati uliopita. Sasa watatuhambulia na ku-tufanya watumwa na kuchu-kua punda wetu!”^b

19 Kwa hiyo wakamfikia msimamizi wa nyumba ya Yo-sefu, wakaongea naye kwe-nye mlango wa nyumba hiyo. **20** Wakamwambia: “Samaha-ni, bwana wetu! Tulikuja huku chini mara ya kwanza kunu-nua chakula.^c **21** Lakini tuli-pofika mahali tulipokuwa tu-kilala na kuanza kufungua mi-fuko yetu, tazama, kila mmoja wetu alikuta pesa zake kwe-nye mdomo wa mfuko wake, kiasi kilekile tulicholeta.^d Basi tungependa kuzirudisha sisi wenyewe. **22** Nasi tumeleta pesa zaidi za kununua cha-kula. Hatujui ni nani aliyewe-ka pesa zetu katika mifuko yetu.”^e **23** Msimamizi huyo akawaambia: “Ni sawa. Msio-gope. Mungu wenu na Mungu wa baba yenu aliweka hazina katika mifuko yenu. Tayari ni-mepokea pesa zenu.” Baada ya hayo akamtoa Simeoni na kumleta kwao.^f

24 Kisha msimamizi huyo akawapeleka ndani ya nyu-mba ya Yosefu, akawapa maji ya kunawa miguu na kuwapa punda wao chakula. **25** Nao wakatayarisha zawa-di^g ya kumpa Yosefu ataka-pokuja mchana, kwa sababu

walisikia kwamba wangekula chakula humo.^a **26** Yosefu alipoingia nyumbani, wakampelekea zawadi yao na kuitama kifudufudi mbele yake.^b **27** Kisha akawauliza kuhusu hali yao na kusema: “Baba yenu aliyezeeka mliyeniambia habari zake anaendeleaje? Je, angali hai?”^c **28** Wakamjibu: “Baba yetu ambaye ni mtumishi wako ni mzima. Angali hai.” Kisha wakainama chini na kuanguka kifudufudi.^d

29 Alipoinua macho yake na kumwona Benjamini ndugu yake, mwana wa mama yake,^e akasema: “Je, huyu ndiye ndugu yenu mdogo mliyeniambia habari zake?”^f Kisha akamwambia: “Mungu na akupe kibali chake, mwanaangu.” **30** Halafu Yosefu akatoka nje haraka kwa sababu alilemewa na hisia alipomwona ndugu yake, akatafuta mahali pa kulilia. Kwa hiyo akaingia katika chumba cha faragha na kulia huku akitokwa na machozi.^g **31** Kisha akanawa uso na kutoka chumbani, sasa akiwa amedhibiti hisia zake, akasema: “Leteni chakula.” **32** Basi wakampa Yosefu chakula chake na ndugu zake chakula chao, nao Wamisri waliokuwa pamoja naye wakala peke yao kwa sababu Wamisri hawangeweza kula pamoja na Waebrania, kwa sababu hilo ni jambo linalochukiza kwa Wamisri.^h

33 Ndugu zake waliketi mbele yake, mzaliwa wa kwanza kulingana na haki yake ya mzaliwa wa kwanzaⁱ na yule mdogo kulingana na umri wake, nao walikuwa wakitazamana kwa mshangao. **34** Yosefu alikuwa akiagiza chaku-

SURA YA 43

a Mwa 43:16

b Mwa 37:7, 9
Mwa 42:6

c Mwa 43:7

d Mwa 37:7, 9

e Mwa 35:24

f Mwa 42:13

g Mwa 42:23, 24

h Mwa 46:33, 34
Kut 8:26

i Mwa 49:3
Kum 21:17

Safu ya 2

a Mwa 45:22

SURA YA 44

b Mwa 42:25

c Mwa 43:12

la kichukuliwe kutoka kwenye meza yake na kupelekwa kwenye meza yao, lakini aliongeza chakula cha Benjamini mara tano zaidi ya chakula ambacho wengine wote walipewa.^a Basi wakaendelea kula na kunywa pamoja naye mpaka waliposhiba.

44 Baadaye Yosefu akamwamuru hivi msimamizi wa nyumba yake: “Ijaze mifuko ya watu hawa kiasi cha chakula wanachoweza kubeba, na uweke pesa za kila mmoja wao katika mdomo wa mfuko wake.^b **2** Lakini kiweke kile kikombe changu, kikombe changu cha fedha, katika mdomo wa mfuko wa yule mdogo, pamoja na pesa zake za nafaka.” Basi akafanya kama Yosefu alivyoagiza.

3 Asubuhi kulipopambazuka, wanaume hao waliruhusiwa kuondoka pamoja na punda wao. **4** Kabla hawajafika mbali kutoka jijini, Yosefu akamwambia yule msimamizi wa nyumba yake: “Ondoka! Wafuatie haraka wanaume hao! Utakapowafikia, waulize, ‘Kwa nini mmelipa uovu kwa wema?’ **5** Je, hiki si kikombe anachotumia bwana wangu kunywea na kukitumia kusoma kwa ustadi ishara za ubashiri? Jambo mlilotenda ni ovu.”

6 Basi msimamizi huyo akawafikia na kuwaambia maneno hayo. **7** Lakini wakamwambia: “Kwa nini bwana wetu unasema jambo kama hili? Sisi watumishi wako hatuwezi kamwe kuwazia kufanya jambo lolote kama hilo. **8** Kwa kweli, pesa tulizopata kwenye midomo ya mifuko yetu tulikurudishia kutoka katika nchi ya Kanaani.^c

Basi tungewezaje kuiba fedha au dhahabu katika nyumba ya bwana wako? **9** Yeyote kati ya watumwa wako atakayepatikana nacho, na auawe, na sisi wengine tutakuwa pia watumwa wa bwana wako.” **10** Kwa hiyo akasema: “Na iwe kama mlivyo-sema: Yule atakayepatikana nacho atakuwa mtumwa wangu, lakini ninyi wengine hamtakuwa na hatia.” **11** Basi kila mmoja akaushusha chini upesi mfuko wake na kuu-fungua. **12** Akaipekua mifuko hiyo kwa makini, akianza na mfuko wa yule mkubwa na kumalizia na mfuko wa yule mdogo. Hatimaye kikombe hicho kikapatikana katika mfuko wa Benjamini.^a

13 Ndipo wakayararua mavazi yao, na kila mmoja akamtwika punda wake mfuko wake, wakarudi jijini. **14** Yuda^b na ndugu zake walipoingia katika nyumba ya Yosefu, bado alikuwemo; nao wakajianguka chini mbele yake.^c **15** Yosefu akawauliza: “Ni jambo gani hili mli-lofanya? Je, hamkujua kwamba mtu kama mimi anaweza kusoma kwa ustadi ishara za ubashiri?”^d **16** Yuda akamjibu: “Tukuambie nini bwana wetu? Tuseme nini? Tutathibitisha jinsi gani kwamba sisi ni waadilifu? Mungu wa kweli amefichua kosa letu sisi watumwa wako.^e Sasa sisi ni watumwa wako bwana wetu, sisi na yule aliyepatikana na kikombe hicho!” **17** Lakini akawaambia: “Siwezi kamwe kuwazia kufanya hivyo! Mtu aliyepatikana na kikombe hicho ndiye atakayekwa mtumwa wangu.^f Lakini ninyi wengine,

SURA YA 44

a Mwa 44:2

b Mwa 43:8
Mwa 44:32

c Mwa 37:7,9

d Mwa 44:5

e Mwa 37:18, 28
Mwa 42:21, 22

f Mwa 44:9

Safu ya 2

a Mwa 41:44
Mwa 45:8b Mwa 42:13
Mwa 43:7

c Mwa 37:31-34

d Mwa 35:18, 19

e Mwa 42:15
Mwa 43:29

f Mwa 42:38

g Mwa 42:20

h Mwa 43:2

i Mwa 43:5

j Mwa 29:18
Mwa 30:22-24
Mwa 35:18, 19
Mwa 46:19

pandeni kwa amani mwende zenu kwa baba yenu.”

18 Sasa Yuda akamkaribia na kumwambia: “Nakushihi, bwana wangu, tafadhali niruhusu mimi mtumwa wako nikwambie neno moja bwana wangu, wala usinikasirikie mimi mtumwa wako, kwa maana wewe ni kama Farao.^a **19** Bwana wangu ulituuliza sisi watumwa wako, ‘Je, mna baba au ndugu?’ **20** Bwana wangu tukakua-ambia, ‘Tuna baba aliyezee-ka na mtoto aliyemzaa uzee-ni, yule mdogo.^b Lakini ndugu yake alikufa,^c kwa hiyo ndiye mwana pekee aliyebaki wa mama yake,^d na baba yake anampenda.’ **21** Kisha ukatuambia sisi watumwa wako, ‘Mleteni huku chini ili nimwone.’^e **22** Lakini bwana wangu tukakwambia, ‘Mvulana huyo hawezi kumwacha baba yake. Akimwacha, kwa hakika baba yake atakufa.’^f **23** Kisha ukatuambia sisi watumwa wako, ‘Ndugu yenu mdogo asiposhuka huku pamoja nanyi, hamtauona uso wangu tena.’^g

24 “Basi tukapanda kwen-nda kwa mtumwa wako, baba yetu, na kumwambia maneno yako bwana wangu. **25** Baadaye baba yetu akatuambia, ‘Rudini huko mkatununulie chakula kidogo.’^h **26** Lakini tukamwambia, ‘Hatuwezi kushuka huko. Tutashuka ikiwa ndugu yetu mdogo atakuwa pamoja nasi, kwa sababu hatuwezi kuuona uso wa mtu huyo ndugu yetu mdogo asipokuwa pamoja nasi.’ⁱ **27** Kisha mtumwa wako baba yetu akatuambia, ‘Mnajua vizuri kwamba mke wangu alinizalia wana wawili tu.’^j

28 Lakini mmoja wao aliniacha, nikasema: “Kwa hakika mnyama wa mwituni amemrua vipandevipande!”^a nami sijamwona mpaka sasa. **29** Mkimchukua huyu pia nisimwone, kisha apatwe na madhara na kufa, hakika mtazishusha mvi zangu Kaburini*^b kwa msiba.^c

30 “Na sasa nikirudi bila mvulana huyu kwa mtumwa wako baba yangu, kwa kuwa uhai wake umefungamana na uhai wa* mvulana huyu, **31** basi mara tu atakapoona mvulana huyu hayupo, atakufa, na kwa kweli sisi watumwa wako tutazishusha mvi za mtumwa wako baba yetu Kaburini* kwa huzuni. **32** Mimi mtumwa wako nilijitoa kuwa dhamana kwa baba yangu kwa ajili ya mvulana huyu, kwa kumwambia, ‘Nisipomrudisha kwako, nitakuwa nimekutendea dhambi milele baba yangu.’^d **33** Basi sasa tafadhali, acha niwe mtumwa wako bwana wangu badala ya mvulana huyu, ili arudi pamoja na ndugu zake. **34** Nitarudije kwa baba yangu bila mvulana huyu? Siwezi kustahimili kuona msiba huo ukimpata baba yangu!”

45 Ndipo Yosefu akashindwa kujizulia mbele ya watumishi wake wote.^e Basi akasema kwa sauti kubwa: “Mwondoeni kila mtu mbele yangu!” Hakuna yeyote aliyebaki pamoja na Yosefu alipokuwa akijitambulisha kwa ndugu zake.^f

2 Kisha akaanza kulia kwa sauti kubwa hivi kwamba Wa-

44:29, 31 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 44:30 *Au “nafsi yake imefungamana na nafsi ya.”

SURA YA 44

a Mwa 37:33

b Zb 16:10
Mhu 9:10
Ho 13:14
Mdo 2:27
Ufu 20:13

c Mwa 37:34, 35
Mwa 42:38
Zb 88:3

d Mwa 43:9

SURA YA 45

e Mwa 43:30

f Mdo 7:13

Safu ya 2

a Mwa 37:28
Mdo 7:9

b Mwa 47:23, 25
Mwa 50:20
Zb 105:17

c Mwa 41:30
Mwa 47:18

d Mwa 46:26

e Zb 105:21
Mdo 7:9, 10

f Mwa 45:26

g Mdo 7:14

h Mwa 46:33, 34
Mwa 47:1
Kut 8:22
Kut 9:26

misri wakamsikia na watu wa nyumba ya Farao wakamsikia. **3** Mwishowe Yosefu akawaambia ndugu zake: “Mimi ni Yosefu. Je, baba yangu angali hai?” Lakini ndugu zake wakashindwa kabisa kumjibu, kwa sababu walishtuka sana kusiakia hivyo. **4** Basi Yosefu akawaambia ndugu zake: “Tafadhali, nikaribieni.” Basi waka mkaribia.

Kisha akawaambia: “Mimi ni Yosefu ndugu yenu, mliyemuza Misri.^a **5** Lakini sasa msikasirike wala kulaumiana kwa kuniuza huku; kwa sababu Mungu alinituma huku niwatangulie ili kuochoa uhai.^b **6** Huu ni mwaka wa pili wa njaa kali nchini,^c na bado kuna miaka mitano ambayo watu hawataweza kulima wala kuvuna. **7** Lakini Mungu alinituma niwatangulie ili niwahifadhi ninyi wazao watakaobaki^d duniani* na ili mwendelee kuwa hai kupitia ukombozi mkubwa. **8** Hivyo basi, si ninyi mliniituma hapa, bali ni Mungu wa kweli, ili aniweke kuwa mshauri mkuu* wa Farao na msimamizi wa nyumba yake yote na mtawala wa nchi yote ya Misri.^e

9 “Rudini upesi kwa baba yangu, mkamwambie, ‘Mwana wako Yosefu amesema hivi: “Mungu ameniweka kuwa msimamizi wa nchi yote ya Misri.^f Shuka uje kwangu. Usikawie.^g **10** Utaishi katika nchi ya Gosheni,^h utakuwa karibu nami—wewe, wana wako, wajukuu wako, makundi yako, mifugo yako, na kila kitu ulicho nacho. **11** Nitakupaa chakula

45:7 *Au “nchini.” 45:8 *Tnn., “kuwa kama baba.”

huko, kwa maana bado kuna miaka mitano ya njaa kali.^a La sivyo, utakuwa maskini, wewe na nyumba yako na kila kitu ulicho nacho.” **12** Ninyi pamoja na ndugu yangu Benjamini mnajionea wenyewe kwamba kwa kweli ni mimi ninayezungumza nanyi.^b

13 Kwa hiyo mnapaswa kumwambia baba yangu kuhusu utukufu wangu wote nchini Misri na kila kitu mlichoona. Sasa fanyeni haraka mkamteremshe huku baba yangu.”

14 Kisha akamkumbatia* Benjamini ndugu yake na kuanza kulia, naye Benjamini akalia huku akiwa amemkumbatia shingoni.^c **15** Akawabusi ndugu zake wote na kuwalia, kisha ndugu zake wakaoonea naye.

16 Habari hizi zikafika katika nyumba ya Farao: “Ndugu za Yosefu wamekuja!” Habari hizo zikamfurahisha Farao na watumishi wake. **17** Basi Farao akamwambia Yosefu: “Waambie ndugu zako, ‘Fanyeni hivi: Watwikeni mizigo wanyama wenu wanaobeba mizigo, mwende katika nchi ya Kanaani, **18** mkamchukue baba yenu na familia zenu mje kwangu. Nitawapa vitu vizuri vya nchi ya Misri, nanyi mtakula* sehemu bora kabisa ya# nchi.^d **19** Nami nakuamuru uwaambie:° ‘Fanyeni hivi: Chukueni magari ya kukokotwa^f kutoka katika nchi ya Misri ya kuwabeba watoto wenu na wake zenu, nanyi mnapaswa kutumia gari moja kumleta baba yenu.^g **20** Msi-

45:14 *Tnn., “akamwangukia shingoni.”

45:18 *Au “mtaishi kwa kutegemea.”

#Au “sehemu nono ya.”

SURA YA 45

a Mwa 47:12

b Mwa 42:23

c Mwa 46:29

d Mwa 47:6

e Mwa 41:39, 40

f Mwa 45:27
Mwa 46:5

g Mwa 47:9

Safu ya 2

a Mwa 46:6

b Mwa 43:34

c Mwa 42:21, 22

d Zb 105:21

e Mwa 42:38
Mwa 44:27, 28

f Mwa 46:30

SURA YA 46

g Mwa 21:31

h Mwa 31:42

Kut 3:6

jali kuhusu mali zenu,^a kwa sababu sehemu bora katika nchi yote ya Misri ni yenu.”

21 Basi wana wa Israeli wakafanya hivyo, naye Yosefu akawapa magari ya kukokotwa kama Farao alivyoamuru, pia akawapa vyakula kwa ajili ya safari. **22** Akampa kila mmoja wao nguo ya kubadili, lakini akampa Benjamini vipande 300 vya fedha na nguo tano za kubadili.^b **23** Naye akamtumia baba yake vitu vi-fuatavyo: punda kumi waliobeba vitu vizuri vya Misri na punda majike kumi waliobeba nafaka na mikate na vyakula vingine kwa ajili ya safari yake. **24** Basi akawaaga ndugu zake, na walipokuwa wakiondoka akawaambia: “Msi-gombane njiani.”^c

25 Basi wakapanda kutoka Misri na kufika katika nchi ya Kanaani kwa Yakobo baba yao. **26** Wakamwambia: “Yosefu angali hai, na ndiye mtawala wa nchi yote ya Misri!”^d Lakini moyo wake ukafa ganzi kwa sababu hakuwaamini.^e **27** Walipoendelea kumwambia mambo yote ambayo Yosefu aliwaambia na alipoona magari ya kukokotwa ambayo Yosefu aliwapa ili yambebe, roho ya Yakobo baba yao ikainza kuhuika. **28** Israeli akasema kwa mshangao: “Inatosh! Yosefu mwanangu angali hai! Ni lazima niende kumwona kabla sijafa!”^f

46 Basi Israeli akachukua kila kitu alichokuwa nacho* na kuondoka. Ali-pofika Beer-sheba,^g alimtolea dhabihu Mungu wa Isaka, baba yake.^h **2** Kisha Mungu

46:1 *Au “watu wake wote.”

akaongea na Israeli katika maono usiku na kumwambia: “Yakobo, Yakobo!” naye akajibu: “Mimi hapa!” **3** Akamwambia: “Mimi ndiye Mungu wa kweli, Mungu wa baba yako.^a Usiogope kushuka kwenenda Misri, kwa maana huko nitakufanya uwe taifa kubwa.^b **4** Mimi mwenyewe nitashuka pamoja nawe Misri, na pia mimi mwenyewe nitakurudisha kutoka huko,^c na Yosefu atayafumba macho yako kwa mkono wake.”^{*d}

5 Kisha Yakobo akaondoka Beer-sheba, na wanawe^{*} wakamsafirisha Yakobo baba yao na watoto wao na wake zao katika magari ya kukokotwa ambayo Farao alikuwa amewapa ili yamsafirishe. **6** Wakachukua mifugo yao na mali zao, walizokuwa wamekusanya katika nchi ya Kanaani. Basi wakafika Misri, Yakobo na wazao wake wote. **7** Alienda Misri pamoja na wanawe na mabinti zake na wajukuu wake wa kiume na wa kike—wazao wake wote.

8 Sasa haya ndiyo majina ya wana wa Israeli waliokuja Misri,^e Yakobo na wanawe: mzaliwa wa kwanza wa Yakobo alikuwa Rubeni.^f

9 Wana wa Rubeni walikuwa Hanoki, Palu, Hezroni, na Karmi.^g

10 Wana wa Simeoni^h walikuwa Yemueli, Yamini, Ohadi, Yakini, Zohari, na Shauliⁱ mwana wa mwana-mke Mkanaani.

11 Wana wa Lawi^j walikuwa Gershoni, Kohathi, na Merari.^k

SURA YA 46

- a Mwa 28:13
- b Mwa 12:1, 2
Kut 1:7
Kum 26:5
- c Mwa 15:16
Mwa 28:15
Mwa 47:29, 30
Mwa 50:13
- d Mwa 50:1
- e Kut 1:1-4
- f Mwa 35:23
1Nya 5:1
- g Hes 26:5, 6
- h Mwa 29:33
- i Hes 26:12, 13
1Nya 4:24
- j Mwa 29:34
- k 1Nya 6:16

Safu ya 2

- a Mwa 29:35
Ufu 5:5
- b Mwa 38:2-5
- c Lu 3:23, 33
- d Mwa 38:30
- e Mwa 38:7, 9, 10
- f Hes 26:21
1Nya 2:5
- g Hes 26:23, 24
1Nya 7:1
- h Mwa 30:20
- i Hes 26:26
- j Mwa 30:21
- k Mwa 30:11
- l Hes 26:15-17
- m Mwa 30:13
- n Hes 26:44, 45
- o Mwa 29:24
- p Mwa 30:24
- q Mwa 35:18
- r Mwa 41:50
- s Mwa 41:51
- t Mwa 41:52
- u 1Nya 7:6
- v 1Nya 8:1, 3
- w 1Nya 7:12
- x Hes 26:38-40

12 Wana wa Yuda^a walikuwa Eri, Onani, Shela,^b Perezzi,^c na Zera.^d Lakini Eri na Onani walikufa katika nchi ya Kanaani.^e

Wana wa Perezzi walikuwa Hezroni na Hamuli.^f

13 Wana wa Isakari walikuwa Tola, Puva, Iobu, na Shimroni.^g

14 Wana wa Zabuloni^h walikuwa Seredi, Eloni, na Yahleeli.ⁱ

15 Hao ndio wana wa Lea, aliomzalia Yakobo huko Padan-aramu, kutia ndani Dina binti yake.^j Wanawe na mabinti zake wote walikuwa 33.

16 Wana wa Gadi^k walikuwa Zifioni, Hagi, Shuni, Esboni, Eri, Arodi, na Areli.^l

17 Wana wa Asheri^m walikuwa Imna, Ishva, Ishvi, na Beria, na dada yao aliitwa Sera.

Wana wa Beria walikuwa Heberi na Malkieli.ⁿ

18 Hao ndio wana wa Zilpa,^o kijakazi ambaye Labani alimpa Lea binti yake. Alimzalia Yakobo wana hao: wote walikuwa 16.

19 Wana wa Raheli, mke wa Yakobo, walikuwa Yosefu^p na Benjamini.^q

20 Katika nchi ya Misri, Asenathi^r binti ya Potifera kuhani wa Oni,^{*} alimzalia Yosefu wana hawa: Manase^s na Efraimu.^t

21 Wana wa Benjamin^u walikuwa Bela, Bekeri, Ashbeli, Gera,^v Naamani, Ehi, Roshi, Mupimu, Hupimu,^w na Ardi.^x

22 Hao ndio wana ambao Raheli alimzalia Yakobo: wote walikuwa 14.

46:4 *Yaani, atayafumba Yakobo atakapokufa. 46:5 *Au “wana wa Israeli.”

46:20 *Yaani, Heliopolisi.

23 Mwana* wa Dani^a alikuwa Hushimu.^b

24 Wana wa Naftali^c walikuwa Yahzeeli, Guni, Yezeri, na Shilemu.^d

25 Hao ndio wana wa Bilha, kijakazi ambaye Labani alimpa Raheli binti yake. Alimzalia Yakobo wana hao: wote walikuwa saba.

26 Wazao wote wa Yakobo walioenda Misri pamoja naye walikuwa 66, bila kuhesabu wake wa wanawe.^e

27 Wana wa Yosefu aliowazaa akiwa Misri walikuwa wawili. Watu wote wa nyumba ya Yakobo waliokuja Misri walikuwa 70.^f

28 Yakobo alimtuma Yuda^g atangulie na kumwambia Yosefu kwamba alikuwa njiani kwenda Gosheni. Wali-pofika katika nchi ya Gosheni.^h **29** Yosefu akaagiza gari lake litayarishwe, kisha akaenda kumpokea Israeli baba yake huko Gosheni. Alipokutana na baba yake, mara moja akamkumbatia* na kulia kwa muda.[#] **30** Kisha Israeli akamwambia Yosefu: "Sasa niko tayari kufa; nimeona uso wako na kujua kwamba ungalihai."

31 Ndipo Yosefu akawambia ndugu zake na watu wa nyumba ya baba yake: "Acheni nipande niende kumjulisha Farao,ⁱ 'Ndugu zangu na watu wa nyumba ya baba yangu waliokuwa katika nchi ya Kanaani wamekuja kwangu.'^j **32** Watu hao ni wachu-

46:23 *Tnn., "Wana." Huenda alikuwa na wana wengine ambao majina yao hayatajwi. **46:29** *Tnn., "akamwangukia shingoni." #Au "na kumlilia shingoni tena na tena."

SURA YA 46

a Mwa 30:6

b Hes 26:42

c Mwa 30:8

d Hes 26:48, 49

e Mwa 35:10, 11

f Kut 1:5
Kum 10:22
Mdo 7:14g Mwa 43:8
Mwa 44:18h Mwa 45:10
Mwa 47:1

i Mwa 41:39, 40

j Mwa 45:19
Mdo 7:13

Safu ya 2

a Mwa 31:17, 18
Mwa 47:3

b Mwa 31:38

c Mwa 46:6

d Mwa 30:35, 36

e Mwa 45:17, 18
Mwa 47:27

f Mwa 43:32

SURA YA 47

g Mwa 46:31

h Mwa 45:10
Kut 8:22

i Mdo 7:13

j Mwa 12:16
Mwa 26:12, 14
Mwa 31:17, 18
Mwa 46:33, 34k Mwa 15:13
Kum 26:5
Zb 105:23
Mdo 7:6

l Mdo 7:11

m Mwa 45:10

n Mwa 45:17, 18

ngaji^a na wafugaji,^b nao wamekuja na kondoo wao na ng'ombe wao na kila kitu walicho nacho.^c **33** Farao akiwaita na kuwauliza, 'Mnafanya kazi gani?' **34** Mnapaswa kumwambia, 'Sisi watumishi wako tumekuwa wafugaji tangu tulipokuwa vijana mpaka sasa, sisi pamoja na mababu zetu,'^d ili mwishi katika nchi ya Gosheni,^e kwa sababu Wamisri wanamchukia kila mtu anayefuga kondoo.^f

47 Basi Yosefu akaenda na kumwambia Farao:^g "Baba yangu na ndugu zangu wamekuja kutoka katika nchi ya Kanaani wakiwa na kondoo wao na ng'ombe wao na mali zao zote, wako katika nchi ya Gosheni."^h **2** Yosefu akachukua watano kati ya ndugu zake na kuwaleta mbele ya Farao.ⁱ

3 Farao akawauliza ndugu zake: "Mnafanya kazi gani?" Wakamjibu: "Sisi watumishi wako ni wafugaji wa kondoo, sisi na mababu zetu."^j

4 Kisha wakamwambia Farao: "Sisi watumishi wako tumeku-
ja kuishi nchini kama wageni^k kwa sababu hakuna mali-
sho kwa ajili ya mifugo yetu,
kwa kuwa njaa ni kali sana
katika nchi ya Kanaani.^l Basi
tafadhali turuhusu sisi watu-
mishi wako tuishi katika nchi
ya Gosheni."^m **5** Ndipo Farao
akamwambia Yosefu: "Baba
yako na ndugu zako wameku-
ja hapa kwako. **6** Nchi ya
Misri iko mbele yako. Wape
baba yako na ndugu zako se-
hemu bora kabisa ya nchiⁿ ili
waishi humo. Waache waishi
katika nchi ya Gosheni, na
ikiwa unajua wanaume wo-
wote wenye ustadi miongoni

mwao, waweke wasimamie mifugo yangu.”

7 Kisha Yosefu akamleta Yakobo baba yake na kumpeleka mbele ya Farao, naye Yakobo akambariki Farao. **8** Farao akamuuliza Yakobo: “Una umri gani?” **9** Yakobo akamwambia Farao: “Nimekuwa nikitangatanga* kwa miaka 130. Miaka yangu imekuwa michache na yenye taabu,^a nayo si mingi kama miaka ambayo mababu zangu waliishi walipokuwa wakitangatanga.”^b **10** Kisha Yakobo akambariki Farao na kutoa mbele yake.

11 Basi Yosefu akawapa makao baba yake na ndugu zake, aliwapa miliki katika nchi ya Misri, katika sehemu bora kabisa ya nchi, katika eneo la Ramesesi,^c kama Farao alivyoamuru. **12** Na Yosefu akaendelea kumpa chakula* baba yake na ndugu zake na watu wote wa nyumba ya baba yake, kulingana na idadi ya watoto wao.

13 Sasa nchi yote haikuwa na chakula* kwa sababu njaa ilikuwa kali sana, basi watu wakadhoofika katika nchi ya Misri na nchi ya Kanaani kwa sababu ya njaa hiyo.^d **14** Yosefu alikuwa akikusanya pesa zote katika nchi ya Misri na nchi ya Kanaani, pesa za nafaka iliyonunuliwa na watu,^e naye alikuwa akizipeleka katika nyumba ya Farao. **15** Hatimaye watu wa nchi ya Misri na nchi ya Kanaani wakaishwa na pesa, na Wamisri wote wakaanza kwenda kwa Yosefu

47:9 *Au “nikihamahama; nikikaa kama mgeni.” ^aAu “wakihamahama; wakikaa kama wageni.” 47:12, 13 *Tnn., “mkate.”

SURA YA 47

a Ayu 14:1, 2

b Mwa 25:7
Mwa 35:28

c Mwa 45:10
Kut 1:8, 11
Kut 12:37
Hes 33:3

d Mwa 41:30, 31

e Mwa 41:56
Mwa 44:25

Safu ya 2

a Mwa 41:48, 49

b Mwa 41:45

na kuwambia: “Tupe chakula! Kwa nini tufe ukituangualia kwa kuwa pesa zetu zimekwisha?” **16** Yosefu akawaambia: “Ikiwa pesa zenu zimekwisha, leteni mifugo yenu, nami nitawapa chakula na kuchukua mifugo yenu.” **17** Basi wakaanza kumletea Yosefu mifugo yao, naye alikuwa akiwapa chakula na kuchukua farasi wao, mifugo yao, na punda wao, na mwaka huo wote alikuwa akiwapa chakula na kuchukua mifugo yao yote.

18 Mwaka huo ulipokwisha, walianza kumjia mwaka uliofuata wakisema: “Hatutakuficha bwana wetu kwamba tumekupa pesa zetu zote na mifugo yetu yote. Hatuna chochote kilichobaki cha kukupa bwana wetu isipokuwa miili yetu na ardhi yetu. **19** Kwa nini tufe ukituangualia, sisi na ardhi yetu? Tununue sisi pamoja na ardhi yetu tupate chakula, nasi pamoja na ardhi yetu tutakuwa watumwa wa Farao. Tupe mbegu ili tuendeleo kuishi, tusife, na ardhi yetu isibaki ukiwa.” **20** Basi Yosefu akamnunulia Farao ardhi yote ya Wamisri, kwa sababu kila Mmisri aliua ardhi yake, kwa maana njaa ilikuwa kali sana; ardhi ikawa mali ya Farao.

21 Kisha akawahamisha watu na kuwapeleka majijini, kutoka mwisho mmoja wa nchi ya Misri mpaka mwisho mwingine.^a **22** Ila tu hakununua ardhi ya makuhani,^b kwa sababu makuhani walipata posho ya chakula kutoka kwa Farao, nao waliishi kwa kutegemea posho waliyopeleka na Farao. Ndiyo sababu

hawakuuza ardhi yao. **23** Kisha Yosefu akawaambia watu: "Tazameni, leo nimewanunua ninyi na ardhi yenu kuwa mali ya Farao. Hapa pana mbegu kwa ajili yenu, zipandeni mashambani. **24** Mtakapopata mavuno, mpeni Farao sehemu ya tano ya mavuno hayo,^a lakini sehemu nne zitakuwa zenu; zitakuwa mbegu za kupanda shambani na chakula chenu na cha watu wa nyumbani mwenu na cha watoto wenu." **25** Basi wakawambia: "Umeokoa uhai wetu.^b Na tupate kibali machoni pako bwana wetu, nasi tutakuwa watumwa wa Farao."^c **26** Kisha Yosefu akai-fanya hiyo kuwa sheria ambayo ingali inafanya kazi nchini Misri hadi leo, kwamba sehemu ya tano ya mavuno ni ya Farao. Ni ardhi ya makuhani tu ambayo haikununuliwa na Farao.^d

27 Waisraeli wakaendelea kuishi Misri, katika nchi ya Gosheni,^e wakakaa humo, nao wakaongezeka na kuwa wengi sana.^f **28** Na Yakobo akae-ndelea kuishi katika nchi ya Misri kwa miaka 17, kwa hiyo siku zote za maisha ya Yakobo zilikuwa miaka 147.^g

29 Wakati wa Israeli kufa ulikuwa ukikaribia,^h kwa hiyo akamwita Yosefu mwanawe na kumwambia: "Ikiwa sasa nimepata kibali machoni pako, tafadhali, weka mkono wako chini ya paja langu, na unitendee kwa upendo mshikamanifu na uaminifu. Tafadhali, usinizike Misri.ⁱ **30** Nitakapokufa,^{*} unapaswa kunibeba na kunitoa Misri na

47:30 *Tnn., "Nitakapolala na baba zangu."

SURA YA 47

a Mwa 41:34

b Mwa 45:5
Mdo 7:11

c Mwa 47:19

d Mwa 47:22

e Mwa 47:4

f Kut 1:7
Kum 10:22
Zb 105:24
Mdo 7:17

g Mwa 47:9

h Mwa 49:33

i Mwa 46:4
Mwa 50:13
Mdo 7:15, 16

Safu ya 2

a Mwa 25:9, 10
Mwa 49:29, 30

b Mwa 50:5

c Ebr 11:21

SURA YA 48

d Mwa 41:50
Yos 14:4e Mwa 28:13, 19
Ho 12:4

f Mwa 35:10, 11

g Mwa 28:13, 14

h Yos 14:4
1Nya 5:1

i Mwa 35:23

j Yos 13:29
Yos 16:5

k Mwa 35:19

l Mik 5:2

m 1Sa 17:12
Mt 2:6

kunizika katika kaburi la mababu zangu."^a Basi Yosefu akasema: "Nitafanya tu kama unavyosema." **31** Kisha Yakobo akasema: "Niapie." Basi akamwapia.^b Ndipo Israeli akainama upande wa kichwa cha kitanda chake.^c

48 Baada ya hayo, Yosefu akaambiwa: "Tazama, baba yako anadhoofika." Basi akawachukua wanawe wawili, Manase na Efraimu, na kwenda nao.^d **2** Ndipo Yakobo akaambiwa: "Tazama, mwana wako Yosefu amekuja kukuona." Basi Israeli akajikakamua na kuketi kitandani. **3** Yakobo akamwambia Yosefu:

"Mungu Mweza-Yote alinitokea kule Luzi katika nchi ya Kanaani na kunibariki.^e **4** Naye akaniambia, 'Ninaku-fanya uzae, nami nitakufanya uwe na watoto wengi, nami nitakufanya uwe kusanyiko la mataifa,^f nami nitau-pa uzao wako* baada yako nchi hii iwe miliki yao ya kudumu.'^g **5** Sasa wana wako wawili uliowazaa katika nchi ya Misri kabla sijaja kwako nchini Misri ni wangu.^h Efraimu na Manase watakuwa wangu kama Rubeni na Simeoni walivyo wangu.ⁱ **6** Lakini watoto utakaowazaa baada yao watakuwa wako. Wataitwa kwa jina la ndugu zao katika urithi wao.^j **7** Nilipokuwa nikitoka Padani, Raheli alikufa^k kando yangu katika nchi ya Kanaani, na bado tulikuwa na safari ndefu kabla ya kufika Efrathi.^l Kwa hiyo nika-mzika huko nikiwa njiani kuelekea Efrathi, yaani, Bethle-hemu."^m

48:4 *Tnn., "nitaipa mbegu yako."

8 Kisha Israeli akawaona wana wa Yosefu na kuuliza: “Ni nani hawa?” 9 Yosefu akamwambia baba yake: “Hawa ni wanangu ambao Mungu amenipa mahali hapa.”^a Yakobo akasema: “Tafadhali walete karibu nami ili niwabariki.”^b 10 Sasa macho ya Israeli yalikuwa yamedhoofika kwa sababu ya uzee, naye hangeweza kuona. Basi Yosefu akawaleta karibu naye, Yakobo akawabusu na kuwakumbatia. 11 Israeli akamwambia Yosefu: “Sikuwazia kamwe kwamba nitauona uso wako,^c lakini sasa Mungu ameniruhusu pia kuona uzao wako.”* 12 Kisha Yosefu akawaondoa kwenye magoti ya Israeli, naye akainama kifudufudi.

13 Halafu Yosefu akawachukua wote wawili na kuwaleta karibu na Yakobo; alimchukua Efraimu^d kwa mkono wake wa kulia na kumweka upande wa kushoto wa Israeli, na Manase^e kwa mkono wake wa kushoto na kumweka upande wa kulia wa Israeli. 14 Lakini Israeli akaunyoo-sha mkono wake wa kulia na kuuweka juu ya kichwa cha Efraimu, ingawa ndiye aliye-kuwa mdogo, halafu akauweka mkono wake wa kushoto juu ya kichwa cha Manase. Aliweka mikono yake hivyo kimakusudi kwa sababu Manase alikuwa mzaliwa wa kwanza.^f 15 Kisha akambariki Yosefu na kusema:^g

“Mungu wa kweli ambaye baba zangu Isaka na Abrahamu walitembea mbele zake,^h

48:11 * Tnn., “mbegu yako.”

SURA YA 48

a Mwa 41:50

b Ebr 11:21

c Mwa 37:34, 35
Mwa 42:36
Mwa 46:30

d Mwa 41:52

e Mwa 41:51

f Mwa 41:51
Mwa 46:20

g 1Nya 5:2

h Mwa 17:1
Mwa 24:40

Safu ya 2

a Mwa 28:13
Zb 23:1

b Mwa 28:15
Mwa 31:11
Zb 34:7

c Mwa 32:26

d Kut 1:7
Hes 26:34, 37

e Mwa 41:51

f Hes 2:18-21

g Hes 1:32, 33

h Ebr 11:21

Mungu wa kweli ambaye amekuwa akinichunga maisha yangu yote mpa-ka leo,^a

16 Malaika ambaye amekuwa akiniponya katika misiba yote,^b awabariki wavulana hawa.^c

Na waitwe kwa jina langu na jina la baba zangu, Abrahamu na Isaka,

Acha waongezeke na kuwa umati mkubwa duniani.”^d

17 Yosefu hakufurahi ali-poona baba yake ameuweka mkono wake wa kulia juu ya kichwa cha Efraimu, basi akashika mkono wa baba yake na kujaribu kuuondoa juu ya kichwa cha Efraimu ili auweke juu ya kichwa cha Manase.

18 Yosefu akamwambia baba yake: “Sivyo baba yangu, kwa kuwa huyu ndiye mzaliwa wa kwanza.^e Weka mkono wako wa kulia juu ya kichwa chake.”

19 Lakini baba yake akazidi kukataa na kusema: “Najua, mwanangu, najua. Yeye pia atakuwa mkuu. Hata hivyo, ndugu yake mdogo atakuwa mkuu kuliko yeye,^f na uzao wake utalingana* kabisa na mataifa.”^g 20 Basi akaendelea kuwabariki siku hiyo,^h akisema:

“Waisraeli na walitaje jina lenu wanapotangaza barama, wakisema,

‘Mungu na awafanye muwe kama Efraimu na kama Manase.’”

Hivyo akaendelea kumtanguliza Efraimu mbele ya Manase.

21 Kisha Israeli akamwambia Yosefu: “Tazama, nina-

48:19 * Tnn., “mbegu yake italingana.”

kufa,^a lakini kwa hakika Mungu ataendelea kuwa pamoja nanyi na kuwarudisha katika nchi ya mababu zenu.^b **22** Mimi ninakupa sehemu moja zaidi ya nchi* kuliko ndugu zako, ambayo nilichukua kutoka mikononi mwa Waamori kwa upanga wangu na upinde wangu.”

49 Basi Yakobo akawaita wanawe na kuwaambia: “Kusanyikeni pamoja niwaambie yatakayowapata katika kipindi cha mwisho cha zile siku. **2** Kusanyikeni msikilize, enyi wana wa Yakobo, naam, msikilizeni Israeli baba yenu.

3 “Rubeni,^c wewe ndiye mzaliwa wangu wa kwanza,^d nguvu zangu na mwanzo wa nguvu zangu za uzazi, ubora wa heshima na ubora wa nguvu. **4** Kwa vurugu kama maji yenye msukosuko, hutafanikiwa, kwa sababu ulikipanda kitanda cha baba yako.^e Wakati huo ulikichafua* kitanda changu. Kwa kweli alikipanda kitanda changu!

5 “Simeoni na Lawi ni ndugu.^f Silaha za ukatili ndizo silaha zao za kuchinjia.^g

6 Usijiunge nao, Ee nafsi* yangu. Usijiunge na kusanyiko lao, Ee heshima yangu.^h kwa sababu kwa hasira yao waliwaua wanaume,^h nao wakawakata ng’ombe dume mishi pa ya miguu ili kujifurahisha. **7** Na ilaaniwe hasira yao, kwa sababu ni katili, na ghadhabu yao, kwa sababu ni kali.ⁱ Acheni niwatawanye katika Yako-

48:22 *Au “mteremko mmoja zaidi wa nchi.” Tnn., “bega moja zaidi.” **49:4** *Au “ulikitia unajisi.” **49:6** *Angalia Kamusi, uku. 2012. ^aAu labda, “mtazamo wangu.”

SURA YA 48

a Mwa 50:24

b Mwa 15:14
Mwa 26:3
Kum 31:8

SURA YA 49

c Kum 33:6

d Mwa 29:32
Kut 6:14
1Nya 5:1

e Mwa 35:22

f Mwa 29:33, 34
Mwa 35:23

g Mwa 34:25

h Mwa 34:7

i Mwa 34:25

Safu ya 2

a Yos 19:1
Yos 21:41b Mwa 29:35
Kum 33:7c Mwa 43:8, 9
Mwa 46:28
1Nya 5:2

d Amu 1:2

e Hes 10:14
2Sa 5:3

f Ufu 5:5

g Hes 24:17
2Sa 2:4
2Sa 7:16, 17h Isa 9:6
Eze 21:27
Lu 1:32
Ebr 7:14i Zb 2:8
Isa 11:10
Mt 2:6

j Kum 33:18, 19

k Mt 4:13

l Yos 19:10

m Kum 33:18
1Nya 7:5

n Kum 33:22

o Amu 13:2, 24
Amu 15:20

bo, na acheni niwasambaze katika Israeli.^a

8 “Nawe Yuda,^b ndugu zako watakusifu.^c Mkono wako utakuwa shingoni mwa maa-dui wako.^d Wana wa baba yako watainama chini mbele yako.^e **9** Yuda ni mwanasimba.^f Mwanangu, kwa haki-ka utapanda juu kutoka mawindoni. Amejikunyata chini na kujinyoosha kama simba, na kama simba, ni nani anayethubutu kumwamsha? **10** Fimbo ya ufalme haitaondoka Yuda,^g wala fimbo ya kiongozi kutoka katikati ya miguu yake, mpaka Shilo* atakapokuja,^h na mataifa yatamtii.ⁱ

11 Atamfungua punda wake kwenye mzabibu na mwana-punda dume wake kwenye mzabibu bora, naye atafua nguo zake katika divai na vazi lake katika damu ya zabibu. **12** Macho yake ni mekundu sana kwa sababu ya divai, na meno yake ni meupe kwa sababu ya maziwa.

13 “Zabuloni^j atakaa kwenye ufuwo wa bahari, kwenye ufuwo ambapo meli hutia nanga,^k na mpaka wake wa mbali utaelekea Sidoni.^l

14 “Isakari^m ni punda mwenye mifupa migumu, aliyelala chini kati ya mizigo miwili aliyobeba. **15** Naye atao-na kwamba mahali pa kupumzikia ni pazuri na kwamba nchi inapendeza. Atainamisha bega lake ili abebe mzigo, naye atakubali kufanya kazi ya utumwa.ⁿ

16 “Dani^o atawahukumu watu wake akiwa mmoja wa makabila ya Israeli.^o **17** Dani

49:10 *Maana yake “Yule Ambaye Ni Yake; Yule Ambaye Ni Mali Yake.”

na awe nyoka kando ya barabara, nyoka mwenye pembe kando ya njia, anayeuma visigino vya farasi na kumwangusha nyuma mpendaji wake.^a **18** Nitasubiri wokovu kutoka kwako, Ee Yehova.

19 "Naye Gadi^b atavamiwa na kundi la wavamizi, lakini atawavamia kwenye visigino vyao.^c

20 "Mkate wa Asheri^d utakuwa mwingi sana,* naye ataandaa chakula kinachomfaa mfalme.^e

21 "Naftali^f ni paa jike mwebamba. Anasema maneno yanayovutia sana.^g

22 "Yosefu^h ni chipukizi la mti unaozaa matunda mengi, mti ulio kando ya chemchemi unaozaa matunda mengi, wenyewe matawi yanayoenea juu ya ukuta. **23** Lakini wapiga mishale waliendelea kumshambulia na kumpiga kwa mishale na kuendelea kuwa na uadui dhidi yake.ⁱ **24** Lakini bado upinde wake ulibaki mahali pake,^j na mikono yake ikaendelea kuwa na nguvu na myepesi.^k Alitiwa nguvu na mikono ya mwenye nguvu wa Yakobo, mchungaji, jiwe la Israeli. **25** Anataka* kwa Mungu wa baba yako, naye atakusaidia, naye yuko pamoja na Mweza-Yote, atakubariki kwa baraka za mbingu zilizo juu, kwa baraka za vilindi vilivyo chini,^l kwa baraka za matiti na tumbo la uzazi. **26** Baraka za baba yako zitakuwa bora kuliko baraka za milima ya milele, bora kuliko vitu vyenye kutamanika vya vilima vinavyodumu.^m Zi-

49:20 *Au "Chakula cha Asheri kitakuwa kingi sana." **49:25** *Yaani, Yosefu.

SURA YA 49

a Amu 14:19
Amu 15:15

b Kum 33:20

c Yos 13:8

d Kum 33:24

e 1Fa 4:7,16

f Kum 33:23

g Mt 4:13,15

h Kum 33:13-17

i Mwa 37:5, 8
Mwa 40:15

j Mwa 50:20

k Yos 1:1, 6
Amu 11:32

l Kum 33:13

m Yos 17:14

Safu ya 2

a Kum 33:16

b Kum 33:12

c Amu 20:15, 16
1Sa 9:16

d Est 2:5
Est 8:7

e Ebr 11:21

f Mwa 35:29
Mwa 49:33

g Mwa 23:17, 18

h Mwa 23:2, 19
Mwa 25:9, 10

i Mwa 35:29

j Mwa 23:17, 18

k Mdo 7:15

SURA YA 50

l Mwa 46:4

taendelea kuwa juu ya kichwa cha Yosefu, juu ya utosi wa kichwa cha yule aliyechaguliwa kutoka kati ya ndugu zake.^a

27 "Benjamini^b ataendelea kurarua kama mbwamwitu.^c Asubuhi atakula mawindo, na jioni atagawanya nyara."^d

28 Hayo yote ndiyo makabila 12 ya Israeli, na hivyo ndivyo baba yao alivyowaambia alipokuwa akiwabariki. Alimpa kila mmoja wao baraka inayomfaa.^e

29 Baada ya hayo aliwapa maagizo haya: "Nakaribia kufa."^f Nizikeni pamoja na baba zangu katika pango lililo kwenye shamba la Efroni Mhiti,^g **30** pango lililo katika shamba la Makpela mbele ya Mamre katika nchi ya Kanaani, shamba ambalo Abrahamu alinunua kutoka kwa Efroni Mhiti ili liwe mahali pa kuzikia. **31** Walimzika huko Abrahamu na Sara mke wake,^h Walimzika huko Isakaⁱ na Rebeka mke wake, na huko ndiko nilikomzika Lea. **32** Shamba hilo na pango lililomo lilinunuliwa kutoka kwa wana wa Hethi."^j

33 Basi Yakobo akamaliza kuwapa wanawe maagizo hayo. Kisha akairudisha miguu yake kitandani, akakata pumzi, naye akazikwa pamoja na watu wake.*^k

50 Ndipo Yosefu akamwangukia baba yake,^l akamlilia na kumbusu. **2** Kisha Yosefu akawaamuru watumishi wake, matabibu, wampake baba yake dawa ili asio-

49:29 *Tnn., "Nakusanywa kwa watu wangu." Huu ni msembo wa kishairi unao-rejelea kifo. **49:33** *Tnn., "akakusanywa kwa watu wake." Huu ni msembo wa kishairi unaorejelea kifo.

ze.^a Basi matabibu hao wa-kampaka dawa Israeli, **3** wa-kafanya hivyo kwa siku 40, muda kamili uliotumiwa kupaka dawa, nao Wamisri wakae-ndelea kumlilia kwa siku 70.

4 Siku za kumwombolezea zilipopita, Yosefu akawaambia hivi watu wa makao* ya Farao: "Ikiwa nimepata kibali macho-ni penu, mpeni Farao ujumbe huu: **5** 'Baba yangu aliniapi-sha^b akisema: "Tazama! nina-kufa.^c Nizike katika kaburi lan-gu^d nililochimba katika nchi ya Kanaani."^e Tafadhali, niru-husu nipande kwenda kumzika baba yangu, kisha nitaru-di."^f **6** Farao akajibu: "Nenda ukamzike baba yako kama alivyokuapisha."^f

7 Basi Yosefu akapanda kwenda kumzika baba yake, alienda pamoja na watumishi wote wa Farao, wazee^g wa makao ya Farao na wazee wote wa nchi ya Misri **8** na watu wote wa nyumba ya Yosefu na ndugu zake na watu wa nyumba ya baba yake.^h Watoto wao wadogo na kondoo wao na ng'ombe wao ndio tu waliobaki katika nchi ya Gosheni. **9** Alienda pia na magariⁱ na wapanda farasi; liliku-wa kundi kubwa sana. **10** Kisha wakafika kwenye uwanja wa kupuria wa Atadi, katika eneo la Yordani, na huko wa-kafanya maombolezo maku-bwa sana na kulia kwa uchungu, naye akaendelea kumwombolezea baba yake kwa siku saba. **11** Wakaaaji wa nchi, Wakanaani, wakawaona wa-kiomboleza kwenye uwanja wa kupuria wa Atadi, wakasema kwa mshangao:

50:4 * Au "nyumba."

SURA YA 50

a Mwa 50:26

b Mwa 47:29-31

c Mwa 48:21

d Mwa 46:4
Mwa 47:29

e Mwa 23:17, 18
Mwa 49:29, 30

f Mwa 47:31

g Zb 105:21, 22

h Mwa 46:27

i Mwa 41:43
Mwa 46:29

Safu ya 2

a Mwa 47:29

b Mwa 23:17, 18
Mwa 25:9, 10
Mwa 35:27
Mwa 49:29, 30

c Mwa 37:18, 28
Mwa 42:21
Zb 105:17

d Mwa 37:7, 9

e Mwa 37:18

"Haya ni maombolezo maku-bwa sana ya Wamisri!" Ndiyo sababu mahali hapo paliitwa Abel-misraimu,* katika eneo la Yordani.

12 Kwa hiyo wana wa Ya-kobo wakamfanyia kama tu alivyokuwa amewaagiza.^a **13** Wanawe walimbeba na kumpeleka katika nchi ya Kanaani na kumzika katika pango lililo katika shamba la Makpela, shamba lililo mbele ya Mamre ambalo Abrahamu alikuwa amenunua kutoka kwa Efroni Mhiti ili awazike humo watu wake.^b **14** Baada ya kumzika baba yake, Yosefu akarudi Misri pamoja na ndugu zake na wote walioenda naye kumzika baba yake.

15 Ndugu za Yosefu wali-poona kwamba baba yao amekufa, wakasema: "Huenda Yosefu ana chuki kutuelekea na atatulipiza uovu wote tulio-ntendea."^c **16** Kwa hiyo wakamtumia Yosefu ujumbe huu: "Baba yako alitoa amri hii kabla ya kifo chake: **17** 'Hivi ndivyo mtakavyomwambia Yosefu: "Nakusihii, tafadhali, wasamehe ndugu zako uovu wao na dhambi waliyokute-ndea ili kukudhuru."^d Sasa, tafadhali, wasamehe watumishi wa Mungu wa baba yako uovu wao." Na Yosefu akalia walipomwambia hivyo. **18** Kisha ndugu zake wakaja pia na kuanguka mbele yake na kumwambia: "Tazama, sisi ni watumwa wako!"^d **19** Yosefu akawaambia: "Msiogope. Je, nimechukua nafasi ya Mungu? **20** Ingawa mlikusudia kunidhuru,^e Mungu alikusudia hali hiyo ibadilike na kuwa

50:11 * Maana yake "Maombolezo ya Wamisri."

njema na kuokoa maisha ya watu wengi, kama anavyofanya leo.^a **21** Sasa basi msio-gope. Nitaendelea kuwapa ninyi na watoto wenu chakula.”^b Kwa hiyo akawafariji na kuwata moyo.

22 Na Yosefu akaendelea kuishi Misri, yeye na watu wa nyumba ya baba yake; Yosefu aliishi miaka 110. **23** Yosefu akaona kizazi cha tatu cha wana wa Efraimu,^c pia wana wa Makiri,^d mwana wa Manasse. Walizaliwa kwenye magoti ya Yosefu.* **24** Mwisho-

50:23 *Yaani, aliwatendea kama wana-we na kwa njia ya pekee.

SURA YA 50

a Mwa 45:5
Zb 105:17

b Mwa 47:12

c 1Nya 7:20

d Yos 17:1
1Nya 7:14

Safu ya 2

a Kut 4:31

b Mwa 12:7
Mwa 17:8
Mwa 26:3
Mwa 28:13

c Kut 13:19
Yos 24:32
Ebr 11:22

d Mwa 50:2

we Yosefu akawaambia ndugu zake: “Ninakufa, lakini kwa hakika Mungu atawakazia uangalifu,^a naye hakika atawapandisha kutoka katika nchi hii na kuwapeleka katika nchi aliyoapa kwamba atawapa Abrahamu, Isaka, na Yakobo.”^b **25** Basi Yosefu akawaapisha wana wa Israeli, akisema: “Kwa hakika Mungu atawakazia ninyi uangalifu. Mnapaswa kuiondoa mifupa yangu huku.”^c **26** Yosefu akafa akiwa na umri wa miaka 110, nao wakampaka dawa ili asioze,^d akawekwa ndani ya jeneza nchini Misri.

KUTOKA

YALIYOMO

- 1 Waisraeli waongezeka Misri (1-7)
Farao awakandamiza Waisraeli (8-14)
Wakunga waliomwogopa Mungu hawakuwaua watoto (15-22)
- 2 Musa azaliwa (1-4)
Binti ya Farao amchukua Musa kuwa mwanawe (5-10)
Musa akimbilia Midiani na kumwoa Sipora (11-22)
Mungu asikia kilio cha chungu cha Waisraeli (23-25)
- 3 Musa na kichaka cha miiba kilichowaka moto (1-12)
Yehova aeleza maana ya jina Lake (13-15)
Yehova ampa Musa maagizo (16-22)
- 4 Ishara tatu ambazo Musa angefanya (1-9)
Musa ahisi hastahili (10-17)
Musa arudi Misri (18-26)
Musa akutana tena na Haruni (27-31)
- 5 Musa na Haruni wakiwa mbele ya Farao (1-5)

- Ukandamizaji wazidi (6-18)
Waisraeli wamlaumu Musa na Haruni (19-23)
- 6 Ahadi ya kuwekwa huru yarudiwa (1-13)
Jina Yehova halikujulikana kikamili (2, 3)
Ukoo wa Musa na Haruni (14-27)
Musa kufika tena mbele ya Farao (28-30)
- 7 Yehova amwimarisha Musa (1-7)
Fimbo ya Haruni yawa nyoka mkubwa (8-13)
Pigo la 1: maji yageuzwa kuwa damu (14-25)
- 8 Pigo la 2: vyura (1-15)
Pigo la 3: mbu (16-19)
Pigo la 4: nzi (20-32)
Nchi ya Gosheni haikuathiriwa (22, 23)
- 9 Pigo la 5: kufa kwa mifugo (1-7)
Pigo la 6: wanadamu na wanyama wapatwa na majipu (8-12)
Pigo la 7: mvua ya mawe (13-35)
Farao ataona nguvu za Mungu (16)
Jina la Yehova litatangazwa (16)

- 10 Pigo la 8: nzige (1-20)
Pigo la 9: giza (21-29)
- 11 Pigo la kumi latangazwa (1-10)
Waisraeli watawaomba Wamisri zawadi (2)
- 12 Kuanzishwa kwa Pasaka (1-28)
Damu itanyunyizwa kwenye miimo ya mlango (7)
Pigo la 10: wazaliwa wa kwanza wauawa (29-32)
Safari ya Kutoka Misri yaanza (33-42)
Miaka 430 yafikia mwisho (40, 41)
Maagizo ya kushiriki Pasaka (43-51)
- 13 Kila mzaliwa wa kwanza wa kiume ni wa Yehova (1, 2)
Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu (3-10)
Kila mzaliwa wa kwanza wa kiume atolewa kwa Mungu (11-16)
Waisraeli waelekezwa kwenye Bahari Nyekundu (17-20)
Nguzo ya wingu na moto (21, 22)
- 14 Waisraeli wafika baharini (1-4)
Farao awafuatia Waisraeli (5-14)
Waisraeli wavuka Bahari Nyekundu (15-25)
Wamisri wazama baharini (26-28)
Waisraeli wawa na imani katika Yehova (29-31)
- 15 Musa na Waisraeli waimba wimbo wa ushindi (1-19)
Miriamu aimba akiwaitikia wanaume (20, 21)
Maji machungu yageuzwa kuwa matamu (22-27)
- 16 Waisraeli wanung'unika kuhusu chakula (1-3)
Yehova asikia manung'uniko yao (4-12)
Wapewa mana na kware (13-21)
Hakuna mana siku ya Sabato (22-30)
Mana yahifadhiwa kuwa ukumbusho (31-36)
- 17 Walalamika kuhusu ukosefu wa maji huko Horebu (1-4)
Maji yatoka mwambani (5-7)
Waamaleki wawashambulia na kuwashinda (8-16)
- 18 Yethro na Sipora wawasili (1-12)
Ushauri wa Yethro wa kuwaweka waamuzi (13-27)
- 19 Kwenye Mlima Sinai (1-25)
- Waisraeli watakuwa ufalme wa makuhani (5, 6)
Watu watakaswa ili wakutane na Mungu (14, 15)
- 20 Amri Kumi (1-17)
Matukio ya ajabu yawaogopesha Waisraeli (18-21)
Maagizo kuhusu ibada (22-26)
- 21 Waisraeli wapewa sheria (1-36)
Kuhusu watumwa Waebrania (2-11)
Kuhusu kumtenda mtu mwingine kwa ukatili (12-27)
Kuhusu wanyama (28-36)
- 22 Waisraeli wapewa sheria (1-31)
Kuhusu wizi (1-4)
Kuhusu kuharibu mazao (5, 6)
Kuhusu kulipia hasara na kumiliki mali (7-15)
Kuhusu kutongoza (16, 17)
Kuhusu ibada na kutenda haki katika jamii (18-31)
- 23 Waisraeli wapewa sheria (1-19)
Kuhusu unyoofu na kutenda wema (1-9)
Kuhusu sabato na sherehe mbalimbali (10-19)
Waisraeli waongozwa na malaika (20-26)
Kuimiliki nchi na mipaka ya nchi (27-33)
- 24 Watu wakubali kushika agano (1-11)
Musa akiwa kwenye Mlima Sinai (12-18)
- 25 Michango kwa ajili ya hema la ibada (1-9)
Sanduku la Agano (10-22)
Meza (23-30)
Kinara cha taa (31-40)
- 26 Hema la ibada (1-37)
Vitambaa vya hema (1-14)
Viunzi na vikalio (15-30)
Mapazia (31-37)
- 27 Madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa (1-8)
Ua (9-19)
Mafuta kwa ajili ya taa (20, 21)
- 28 Mavazi ya kuhani (1-5)
Efodi (6-14)
Kifuko cha kifuanzi (15-30)
Urimu na Thumimu (30)
Joho lisilo na mikono (31-35)

- Kilemba chenye bamba la dhahabu (36-39)
Mavazi mengine ya kuhani (40-43)
- 29 Makuhani wawekwa rasmi (1-37)
Matoleo ya kila siku (38-46)
- 30 Madhabahu ya uvumba (1-10)
Kuhesabiwa kwa watu na pesa za dhahabu ya kufunika dhambi (11-16)
Beseni la shaba la kunawia mikono na miguu (17-21)
Mchanganyiko wa pekee wa mafuta yanayotumiwa kutia mafuta (22-33)
Utaratibu wa kutengeneza uvumba mtakatifu (34-38)
- 31 Mafundi wajazwa roho ya Mungu (1-11)
Sabato, ishara kati ya Mungu na Waisraeli (12-17)
Mabamba mawili ya mawe (18)
- 32 Ibada ya ndama wa dhahabu (1-35)
Musa asikia uimbaji usio wa kawaida (17, 18)
Musa ayavunjavunja mabamba ya sheria (19)
Walawi wabaki washikamanifu kwa Yehova (26-29)
- 33 Mungu awakaripia Waisraeli (1-6)
Hema la mkutano nje ya kambi (7-11)
Musa aomba kuona utukufu wa Yehova (12-23)
- 34 Mabamba mapya ya mawe yatengenezwa (1-4)
- Musa aona utukufu wa Yehova (5-9)
Maagizo kuhusu agano yarudiwa (10-28)
Uso wa Musa watoa miale (29-35)
- 35 Maagizo kuhusu Sabato (1-3)
Michango ya hema la ibada (4-29)
Bezaleli na Oholiabu wajazwa roho (30-35)
- 36 Michango yazidi (1-7)
Ujenzi wa hema la ibada (8-38)
- 37 Kutengeneza sanduku la agano (1-9)
Meza (10-16)
Kinara cha taa (17-24)
Madhabahu ya uvumba (25-29)
- 38 Madhabahu ya dhahabu za kuteketezwa (1-7)
Beseni la shaba (8)
Ua (9-20)
Orodha ya vifaa vya hema la ibada (21-31)
- 39 Kutengeneza mavazi ya kuhani (1)
Efodi (2-7)
Kifuko cha kifuani (8-21)
Joho lisilo na mikono (22-26)
Mavazi mengine ya kuhani (27-29)
Bamba la dhahabu (30, 31)
Musa akagua hema la ibada (32-43)
- 40 Ujenzi wa hema la ibada (1-33)
Utukufu wa Yehova wajaa katika hema la ibada (34-38)

1 Sasa haya ndiyo majina ya wana wa Israeli walioingia Misri pamoja na Yakobo, kila mwanamume aliyekuja na watu wa nyumba yake:^a **2** Rubeni, Simeoni, Lawi, na Yuda;^b **3** Isakari, Zabuloni, na Benjamini; **4** Dani na Naftali; Gadi na Asheri.^c **5** Na wazao wote wa Yakobo* walikuwa 70, lakini tayari Yosefu alikuwa Misri.^d **6** Mwisho-

1:5 *Tnn., "Na wote waliotoka katika kiu-no cha Yakobo."

SURA YA 1

a Mwa 46:8

b 1Nya 2:3, 4

c Mwa 46:17

d Mwa 46:26
Kum 10:22
Mdo 7:14

Safu ya 2

a Mwa 50:26

b Mwa 46:3
Kum 26:5
Mdo 7:17-19

we Yosefu akafa,^a na pia ndugu zake wote na kizazi hicho chote. **7** Na Waisraeli* wakaanza na kuanza kuongezeka sana, nao wakazidi kuwa wengi na kuwa na nguvu isivyo kawaida, hivi kwamba wakaajaa nchini.^b

8 Baada ya muda mfalme mpya ambaye hakumjua Yosefu akaanza kutawala Misri. **9** Akawaambia watu wake: "Tazameni! Waisraeli ni wengi zaidi na wenye nguvu kuliko

1:7 *Tnn., "wana wa Israeli."

sisi.^a **10** Acheni tushughulike nao kwa akili. La sivyo, wataendelea kuongezeka, na vita vikitokea, wataungana na maadui wetu na kupigana nasi na kuondoka nchini.”

11 Basi wakaweka wasimamizi wa kazi za utumwa* ili wawatumikishe na kuwakandamiza kwa kazi ngumu,^b nao wakamjengea Farao majiji yenye maghala, yaani, Pithomu na Raamsesi.^c **12** Lakini kadiri walivyozidi kuwakandamiza, ndivyo walivyozidi kuongezeka na ndivyo walivyozidi kuenea kotekote, kwa hiyo wakaogopa sana na kuchukizwa na Waisraeli.^d **13** Kwa hiyo, Wamisri wakawalazimisha Waisraeli kuwa watumwa na kuwatesa kikatili.^e **14** Wakafanya maisha yao yawe machungu kwa kazi ngumu ya kutengezeka saruji ya udongo wa mfiyanzi na matofali na katika kila aina ya utumwa shambani. Naam, waliwalazimisha wafanye kazi ngumu chini ya hali ngumu sana katika kila aina ya utumwa.^f

15 Baadaye mfalme wa Misri akazungumza na wakungu Waebrania walioitwa Shifra na Pua, **16** akawaambia: “Mnapowasaidia wanawake Waebrania kuzaa,^g wanapokuwa kwenye kiti cha kuzalia, mnapaswa kumuua mtoto huyo ikiwa ni wa kiume; lakini ikiwa ni wa kike, mwacheni aishi.” **17** Hata hivyo, wakungu hao walimwogopa Mungu wa kweli, kwa hiyo hawakufanya kama walivyoambiwa na mfalme wa Misri. Badala yake, waliwaacha watoto wa kiume waishi.^h **18** Baada

1:11 *Au “wasimamizi wa kazi.”

SURA YA 1

a Zb 105:24, 25

b Mwa 15:13

Kut 3:7

Hes 20:15

Kum 26:6

c Mwa 47:11

d Kut 1:7

Zb 105:24, 25

e Kut 2:23

Mdo 7:6

f Law 26:13

g Eze 16:4

h Mwa 9:5, 6

Safu ya 2

a Mdo 7:18, 19

SURA YA 2

b Kut 6:20

Hes 26:59

c Mdo 7:20

Ebr 11:23

d Mdo 7:18, 19

e Kut 15:20

1Nya 6:3

Mik 6:4

ya muda mfalme wa Misri akawaita wakungu hao na kuwauliza: “Kwa nini mmewaacha watoto wa kiume waishi?” **19** Wakungu hao wakamjibu Farao: “Wanawake Waebrania si kama wanawake Wamisri. Wana nguvu nao huzaa kabla mkunga hajafika.”

20 Kwa hiyo Mungu akawatendea mema wakungu hao, na Waisraeli wakazidi kuongezeka na kuwa wenye nguvu sana. **21** Na kwa sababu wakungu hao walimwogopa Mungu wa kweli, baadaye aliwapa familia. **22** Hatimaye Farao akawaamuru hivi watu wake wote: “Mnapaswa kumtupa kwenye Mto Nile kila mtoto mchanga wa kiume anayezaliwa na Waebrania, lakini mtamwacha hai kila mtoto wa kike.”^a

2 Karibu na wakati huo, mwanamume fulani wa nyumba ya Lawi alimwoa binti ya Lawi.^b **2** Mwanamke huyo akapata mimba na kuzaa mwana. Alipoona kwamba mwana huyo ana sura yenye kupendeza sana, alimficha kwa miezi mitatu.^c **3** Aliposhindwa kuendelea kumficha,^d alichukua kikapu cha mafunjo* na kukipaka lami na bereu, akamweka mtoto huyo ndani yake na kukiweka kati ya matete kando ya Mto Nile. **4** Lakini dada ya mtoto huyo^e akasimama mbali kidogo ili aone yata-kayompata ndugu yake.

5 Binti ya Farao aliposhuka kwenye Mto Nile ili kuoga, watumishi wake wa kike walikuwa wakitembeatembea kando ya Mto Nile. Binti ya Farao akaona kikapu hicho kati ya

2:3 *Au “safina; sanduku.”

matete. Mara moja akamtuma kijakazi wake akilete.^a **6** Alipokifungua, alimwona mwana huyo akilia. Akamhurumia, lakini akasema: "Huyu ni mtoto wa Waebrania." **7** Kisha dada ya mtoto huyo akamuuliza binti ya Farao: "Je, niende nikamwite mwanamke mlezi Mwebrania akunyonyeshee mtoto huyu?" **8** Binti ya Farao akamwambia: "Nenda!" Msichana huyo akienda mara moja na kumwita mama ya mtoto huyo.^b **9** Kisha binti ya Farao akamwambia: "Mchukue mtoto huyu uninyonyeshee, nami nitakulipa." Basi mwanamke huyo akamchukua na kumnyonyesha. **10** Mtoto huyo alipokuwa mkubwa kidogo, akamleta kwa binti ya Farao, naye akawa mwanawe.^c Akampa jina Musa* na kusema: "Ni kwa sababu nimemtoa katika maji."^d

11 Siku hizo, baada ya Musa kuwa mtu mzima,* alitoka kwenda kwa ndugu zake ili kuona mizigo waliyokuwa wakibeba,^e akamwona Mmisri akimpiga Mwebrania, mmoja wa ndugu zake. **12** Kwa hiyo Musa akatazama huku na kule, na alipoona kwamba hakuna yeyote, akamuua Mmisri huyo na kumficha mchangani.^f

13 Lakini Musa alitoka siku iliyofuata, akawaona wanau-me wawili Waebrania wakipigana. Basi akamuuliza yule aliyekosea: "Kwa nini unampiga mwenzako?"^g **14** Akasema: "Ni nani aliyekuweka kuwa mkuu na mwamuzi wetu? Je, unapanga kuniua kama ulivyomuua yule Mmi-

2:10 *Maana yake "Aliyetolewa," yaani, aliyeokolewa kutoka katika maji. 2:11 *Au "Musa alipokuwa akipata nguvu."

SURA YA 2

a Mdo 7:21

b Kut 6:20

c Ebr 11:24, 25

d Mdo 7:21

e Kut 1:11

Kut 3:7

Mdo 7:23

f Mdo 7:24

g Mdo 7:26

Safu ya 2

a Mdo 7:27, 28

b Mwa 25:1, 2

Kut 3:1

Kut 4:19

c Kut 18:12

d Kut 4:18

Kut 18:1

Hes 10:29

e Mdo 7:22

f Kut 18:2-4

Hes 12:1

g 1Nya 23:15

h Mdo 7:29

i Kut 7:7

Mdo 7:30

sri?"^a Basi Musa akaogopa na kusema moyoni: "Bila shaka jambo hilo limejulikana!"

15 Kisha Farao akasikia habari hizo, naye akajaribu kumuua Musa; lakini Musa akamkimbia Farao na kwenda kuishi katika nchi ya Midiani;^b alipofika huko akaketi kando ya kisima. **16** Sasa kuhani wa Midiani^c alikuwa na mabinti saba, nao wakaja kuteka maji na kujaza vyombo vya kunywesha kondoo wa baba yao. **17** Lakini kama kawaida, wachungaji walikuja na kuwafukuza mabinti hao. Kwa hiyo Musa akainuka, akawa-saidia* wanawake hao, na kunywesha kondoo wao. **18** Walipofika nyumbani kwa Reueli^{*d} baba yao, akawauliza kwa mshangao: "Mbona mmerudi upesi sana leo?" **19** Wakamjibu: "Mmisri fulani alitukoa kutoka mikononi mwa wachungaji, na hata alitutekea maji na kuwanyesha kondoo." **20** Reueli akawaambia mabinti zake: "Lakini yuko wapi? Kwa nini hamkuja naye? Mwiteni, ili ale chakula pamoja nasi." **21** Baada ya hayo Musa akakubali kuishi na mtu huyo, naye akampa Musa binti yake aliyetitwa Sipora^f ili amwoe. **22** Baadaye Sipora akazaa mwana, naye Musa akamwita mwana huyo Gershomu,^{*g} kwa sababu alisema: "Nimekuwa mkaaji mgeni katika nchi ya kigeni."^h

23 Baada ya muda mrefu,* mfalme wa Misri akafa,ⁱ lakini Waisraeli wakaendelea kulia kwa chungu kwa sababu ya

2:17 *Au "akawatetea." 2:18 *Yaani, Yethro. 2:22 *Maana yake "Mkaaji Mgeni Huko." 2:23 *Tnn., "siku nyingi."

utumwa na kupaza kilio cha malalamishi, na kilio chao cha kuomba msaada kwa sababu ya utumwa kikaendelea kupanda juu kwa Mungu wa kweli.^a **24** Mwishowe Mungu akasiakia kilio chao cha uchungu,^b naye akakumbuka agano lake alilofanya na Abrahamu, Isaka, na Yakobo.^c **25** Basi Mungu akawakazia uangalifu Waisraeli; na Mungu akayaona mateso yao.

3 Musa akawa mchungaji wa kondoo wa Yethro,^d baba mkwe wake, kuhani wa Midiani. Alipokuwa akiwaongoza kondoo kuelekea upande wa magharibi wa nyika, hatimaye alifika kwenye mlima wa Mungu wa kweli ulioitwa Horebu.^e **2** Kisha malaika wa Yehova akamotokea katika mwali wa moto katikati ya kichaka cha miiba.^f Musa alipoendelea kutazama, aliona kwamba kichaka hicho cha miiba kilikuwa kikiwaka moto, lakini hakikuteketea. **3** Basi Musa akasema: "Nitaenda kuchunguza jambo hili la ajabu, nione kwa nini kichaka kile cha miiba hakiteketei." **4** Yehova alipooa akienda kuitazama, Mungu akamwita kutoka katika kichaka cha miiba: "Musa! Musa!" naye akajibu: "Mimi hapa." **5** Akamwambia: "Usikaribie zaidi. Vua viatu vyako, kwa sababu mahali unaposimama ni ardhi takatifu."

6 Akaendelea kusema: "Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu,^g Mungu wa Isaka,^h na Mungu wa Yakobo."ⁱ Ndipo Musa akauficha uso wake, kwa sababu alioogopa kumtazama Mungu wa kweli. **7** Kisha Yehova akasema: "Hakika nimeyaona mate-

SURA YA 2

a Kut 3:7
1Fa 8:51

b Mdo 7:34

c Mwa 15:13, 14
Kut 6:5
Hes 20:15, 16

SURA YA 3

d Kut 2:16
Kut 18:1e Kut 24:12, 13
1Fa 19:8, 9

f Mdo 7:30-34

g Mwa 17:1, 7

h Mwa 26:24

i Mwa 28:13
Mwa 32:9
Mt 22:32
Mdo 7:32

Safu ya 2

a Kut 1:11
Isa 63:9
Mdo 7:34

b Kut 12:51

c Hes 13:26, 27
Kum 27:3d Mwa 10:15-17
Kut 33:1, 2
Kum 7:1
Yos 3:10
Ne 9:7, 8

e Kut 1:11

f Zb 105:26, 38
Mdo 7:34g Kum 31:23
Yos 1:5
Isa 41:10
Ro 8:31
Flp 4:13h Kut 19:2
Kum 4:11, 12i Kut 15:3
Zb 96:8
Zb 135:13
Ho 12:5
Yoh 17:26
Ro 10:13j Ayu 23:13
Isa 14:27
Yoh 12:28

so ya watu wangu walio Misri, nami nimesikia kilio chao kwa sababu ya wale wanaowalazimisha kufanya kazi; ninajua vema maumivu yao.^a **8** Nita-shuka huko ili niwaokoe kutoka mikononi mwa Wamisri^b na kuwapandisha kutoka katika nchi hiyo na kuwapeleka katika nchi nzuri na kubwa, nchi inayotiririka maziwa na asali,^c eneo la Wakanaani, Wahiti, Waamori, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi.^d **9** Sasa tazama! Kilio cha Waisraeli kimenifikia, nami nimeona pia jinsi Wamisri wanavyowakandamiza kwa ukatili.^e **10** Sasa njoo, nitakutuma kwa Farao, nawe utawatoa watu wangu Waisraeli kutoka Misri."^f

11 Hata hivyo, Musa akamwambia Mungu wa kweli: "Mimi ni nani hata niende kwa Farao na kuwatoa Waisraeli nchini Misri?" **12** Mungu akamwambia: "Nitathibitika kuwa pamoja nawe,^g na hii ndiyo ishara itakayoonyesha kwamba ni mimi niliyekutumama: Baada ya kuwatoa Waisraeli nchini Misri, ninyi mtanitumikia* mimi, Mungu wa kweli, kwenye mlima huu."^h

13 Lakini Musa akamwambia Mungu wa kweli: "Tuseme niende kwa Waisraeli na kuwaambia, 'Mungu wa mababu zenu amenituma kwenu,' nao waniulize, 'Jina lake ni nani?'" Niwaambie nini?"

14 Basi Mungu akamwambia Musa: "Nitakuwa Kile Ninachochagua* Kuwa."^j Kisha akasema: "Hivi ndiyo unavyopaswa kuwaambia

3:12 *Au "mtaniabudu." **3:14** *Au "Ninachotaka." [#]Au "Nitathibitika Kuwa Kile Nitakachothibitika Kuwa." Angalia Nyongeza A4.

Waisraeli, 'Nitakuwa amenituma kwenu.'"^a **15** Tena Mungu akamwambia Musa:

"Hivi ndivyo unavyopaswa kuwaambia Waisraeli, 'Yehova Mungu wa mababu zenu, Mungu wa Abrahamu,^b Mungu wa Isaka,^c na Mungu wa Yakobo,^d amenituma kwenu.' Hilo ndilo jina langu milele,^e na hivyo ndivyo ninavyopaswa kukumbukwa kizazi baada ya kizazi. **16** Sasa nenda, uwakusanye wazee wa Israeli na kuwaambia, 'Yehova Mungu wa mababu zenu amenitokea, Mungu wa Abrahamu, Isaka, na Yakobo, naye alisema: "Hakika nimewatazama^f na nimeona mambo mnayotendewa nchini Misri. **17** Kwa hiyo ninasema, nitawatoa katika mateso^g mnayopata mikononi mwa Wamisri na kuwapeleka katika nchi ya Wakanaanani, Wahiiti, Waamori,^h Waperizi,ⁱ Wahiivi, na Wayebusi, nchi inayotiririka maziwa na asali."^j

18 "Hakika wataisikiliza sauti yako,^k nawe utaenda, wewe pamoja na wazee wa Israeli, kwa mfalme wa Misri, nanyi mnapaswa kumwambia: 'Yehova Mungu wa Waebrania' amewasiliana nasi. Kwa hiyo, tafadhali, turuhusu tusafiri kwa siku tatu nyikani ili tumtolee Yehova Mungu wetu dhabihu.'^m **19** Lakini mimi mwenyewe ninajua vema kwamba mfalme wa Misri hatawaruhusu kwenda asipolazimishwa kwa mkono wenye nguvu.ⁿ **20** Kwa hiyo nitalazimika kuunyoosha mkono wangu na kuipiga Misri kwa matendo yangu yote ya ajabu nitakayofanya nchini humo, kisha atawaruhusu mwo-

SURA YA 3

a Kut 6:3, 7
Ro 9:17

b Mwa 17:1, 7

c Mwa 26:24

d Mwa 28:13
Mt 22:32

e Zb 135:13

f Mwa 50:24
Kut 13:19

g Mwa 15:13, 14
Law 26:13

h Mwa 15:16

i Kut 23:23

j Hes 13:27
Kum 8:7-9

k Kut 4:31

l Mwa 14:13

m Kut 5:3
Kut 10:25, 26

n Kut 5:2
Kut 14:8
Ro 9:17

Safu ya 2

a Kut 7:3
Kut 12:33
Kum 6:22

b Kut 11:2
Kut 12:35, 36

c Mwa 15:13, 14
Kut 12:36

SURA YA 4

d Kut 2:13, 14

e Kut 7:9

f Lu 20:37

g Kut 3:16
Kut 4:31

h Hes 12:10

ndoke.^a **21** Nami nitawafanya watu hawa wapate kibali machoni pa Wamisri, nanyi mtakapoondoka, hamtaondoka kamwe mikonu mitupu.^b **22** Kila mwanamke anapaswa kumwomba jirani yake na mwanamke anayeishi nyumbani mwake vito vya fedha na vya dhahabu na pia mavazi, nanyi mtawavika wana wenu na mabinti wenu; nanyi mtachukua mali za Wamisri."^c

4 Hata hivyo, Musa akamwambia: "Lakini tuseme kwamba hawaniamini wala kuisikiliza sauti yangu,^d kwa maana watasema, 'Yehova hakukutokea.'" **2** Ndipo Yehova akamuuliza: "Ni nini hicho kilicho mkononi mwako?" Akajibu: "Fimbo." **3** Akamwambia: "Itupe chini." Basi akaitupa chini, nayo ikawa nyoka;^e Musa akamkimbia. **4** Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Unyooshe mkono wako umkamate mkia." Basi akaunyoosha mkono wake na kumkamata, nyoka huyo akawa fimbo mkononi mwake. **5** Kisha Mungu akamwambia: "Fanya hivyo ili waamini kwamba Yehova Mungu wa mababu zao, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo,^f amekutokea."^g

6 Tena Yehova akamwambia: "Tafadhali, utie mkono wako ndani ya mkunjo wa juu wa vazi lako." Basi akautia mkono wake ndani ya mkunjo wa vazi lake. Alipoutoa, tazama, mkono wake ulikuwa umepigwa na ukoma, ukawa mweupe kama theluji!^h **7** Kisha Mungu akamwambia: "Urudisha mkono wako kwenye mkunjo wa juu wa vazi lako." Basi akaurudisha mko-

no wake ndani ya vazi lake. Alipoutoa katika vazi lake, ulikuwa umerudia hali yake na kuwa kama sehemu nyingine za mwili wake! **8** Mungu akasema: "Wasipokuamini au wakipuuza ishara ya kwanza, basi kwa hakika watatii ishara^a ya pili. **9** Lakini hata wasipoamini ishara hizo mbili na kukataa kuisikiliza sauti yako, utachota maji kutoka katika Mto Nile na kuyamwaga kwenye nchi kavu, na maji hayo yatakuwa damu kwenye nchi kavu."^b

10 Sasa Musa akamwambia Yehova: "Ee Yehova, niwie radhi, lakini sijawahi kuwa msemaji mwenye ufasaha, tangu zamani na hata baada ya wewe kuzungumza nami mtumishi wako, kwa maana mimi si msemaji mzuri* na ulimi wangu ni mzito."^c **11** Yehova akamuuliza: "Ni nani aliyemuambia mwanadamu kinywa, au ni nani anayewafanya wawe bubu, viziwi, waone vizuri, au wawe vipofu? Je, si mimi, Yehova? **12** Basi nenda sasa, nami nitakuwa pamoja nawe utakapokuwa ukizungumza,* nami nitakufundisha unalopaswa kusema."^d

13 Lakini akasema: "Ee Yehova, niwie radhi, tafadhali, mtume yeyote unayetaka kumtuma." **14** Ndipo hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Musa, akasema: "Namna gani ndugu yako Haruni,^e Mlawi? Ninajua kwamba anaweza kuzungumza vizuri sana. Na sasa yuko njiani anakuja hapa kukutana nawe. Atakapokuona, moyo wake utashangilia."^f

4:10 *Tnn., "nina kinywa kizito." 4:12 *Tnn., "nitakuwa na kinywa chako."

SURA YA 4

a Mdo 7:36

b Kut 4:30

c Kut 6:12
Hes 12:3
Yer 1:6
Mdo 7:22d Isa 50:4
Mk 13:11

e Hes 26:59

f Kut 4:27

Safu ya 2

a Kut 4:28

b Yer 1:9

c Kut 7:1, 2

d Kut 8:5
Kut 17:5, 6
Hes 20:11e Kut 2:18, 21
Kut 18:1
Hes 10:29

f Kut 2:15

g Kut 7:9

h Kut 7:3
Kut 8:15
Kut 9:12
Kut 11:10
Ro 9:17, 18

i Kut 7:22

j Kum 7:6
Kum 14:2
Ho 11:1
Ro 9:4

15 Basi unapaswa kuzungumza naye na kuweka maneno hayo kinywani mwake,^a nami nitakuwa pamoja nawe na yeye pia mnapozungumza,^b nami nitawafundisha jambo la kufanya. **16** Atazungumza na watu kwa niaba yako, naye atakuwa msemaji wako, nawe utakuwa kama Mungu kwake.*^c **17** Nawe utachukua fimbo hii mkononi mwako na kuitumia kufanya zile ishara."^d

18 Basi Musa akarudi kwa Yethro baba mkwe wake^e na kumwambia: "Ninataka kwenda, tafadhali, nirudi kwa ndugu zangu walio Misri nione kama wangali hai." Yethro akamwambia Musa: "Nenda kwa amani." **19** Basi Yehova akamwambia Musa huko Midiani: "Nenda, rudi Misri, kwa sababu watu wote waliotaka kukuu* wamekufa."^f

20 Kisha Musa akamchukua mke wake na wanawe na kuwapandisha juu ya punda, akaanza safari ya kurudi nchini Misri. Pia, Musa aliichukua ile fimbo ya Mungu wa kweli mkononi mwake. **21** Halafu Yehova akamwambia Musa: "Baada ya kurudi Misri, haki-kisha kwamba unafanya mbele ya Farao miujiza yote ambayo nimekupa nguvu za kuifanya."^g Lakini nitauacha moyo wake uwe mkaidi,^h naye hatwaruhusu watu hao wao ndoke.ⁱ **22** Unapaswa kumwambia Farao, 'Hivi ndivyo Yehova anavyosema: "Israeli ni mwanangu, mzaliwa wangu wa kwanza."^j **23** Ninakwambia, Mruhusu

4:16 *Au "atakuona kuwa mwakilishi wa Mungu." 4:19 *Au "waliokuwa wakiita-futa nafsi yako."

mwanangu aondoke ili anitumikie. Lakini ukikataa kumruhusu aondoke, nitamuua mwana wako, mzaliwa wako wa kwanza.”^a

24 Sasa walipokuwa njiani, mahali pa kulala, Yehova^b akakutana naye, na alikuwa akita-futa kumuua.^c **25** Hatimaye Sipora^d akachukua jiwe gumu lenye makali* na kumtahiri mwanawe, kisha akagusa miguu yake[#] kwa govi hilo na kusema: “Ni kwa sababu wewe ni bwana harusi wa damu kwangu.” **26** Basi Mungu akamwacha aende. Wakati huo Sipora akasema, “bwana harusi wa damu,” kwa sababu ya tohara hiyo.

27 Kisha Yehova akamwambia Haruni: “Nenda nyikani ukakutane na Musa.”^e Basi akaenda na kukutana naye kwenye mlima wa Mungu wa kweli^f na kumsalimu kwa busu. **28** Na Musa akamwambia Haruni maneno yote ya Yehova, aliyekuwa amemtuma,^g na ishara zote alizomwamuru afanye.^h **29** Kisha Musa na Haruni wakaenda kuwakusanya wazee wote wa Waisraeli.ⁱ **30** Haruni akawaambia maneno yote ambayo Yehova alimwambia Musa, naye akafanya zile ishara/ machoni pa watu. **31** Kwa hiyo watu wakaamini.^k Waliposikia kwamba Yehova alikuwa amewaelekeza uangalifu Waisraeli^l na kwamba alikuwa ameona mateso yao,^m wakainama chini na kusujudu.

5 Baadaye, Musa na Haruni wakaenda kwa Farao na kumwambia: “Hivi ndivyo anavyosema Yehova Mungu

4:25 *Au “kisu cha jiwe gumu.” [#]Labda ni miguu ya malaika.

SURA YA 4

a Kut 12:29

b Hes 22:22
1Nya 21:16

c Mwa 17:14

d Kut 2:16, 21

e Kut 4:14

f Kut 3:1
Kut 20:18
Kut 24:16

g Kut 4:15

h Kut 4:8

i Kut 3:16
Kut 24:1

j Kut 4:3, 6, 9

k Kut 3:18

l Mwa 50:25

m Kut 1:14
Kut 3:7
Kum 26:6

Safu ya 2

SURA YA 5

a Kut 7:5
Kut 9:15, 16

b 2Fa 18:28, 35

c Kut 3:19

d Kut 3:18

e Kut 1:11

f Kut 1:14

g Kut 1:11

wa Israeli, ‘Waruhusu watu wangu waende ili wanifanyie sherehe nyikani.’” **2** Lakini Farao akasema: “Yehova ni nani,^a hivi kwamba nitii sauti yake na kuwaruhusu Waisraeli waende zao?^b Simjui Yehova kamwe, na isitoshe, sitawaruhusu Waisraeli waende zao.”^c **3** Lakini wakamwambia: “Mungu wa Waebrania amewasiliana nasi. Tafadhali, tungependa kusafiri kwa siku tatu kwenda nyikani tukamtolee dhabihu Yehova Mungu wetu;^d tusipofanya hivyo, atatupiga kwa ugonjwa au kwa upanga.” **4** Mfalme wa Misri akawaambia: “Musa na Haruni, kwa nini mnawafanya watu waache kazi zao? Rudini mkafanye kazi yenu!”^e **5** Farao akaendelea kusema: “Angalieni jinsi watu walivyo wengi nchini, nanyi mnataka kuwafanya waache kazi yao.”

6 Siku hiyohiyo, Farao akawaamuru hivi wasimamizi wa kazi na wasimamizi wa watumwa: **7** “Msiwape tena watu hawa nyasi za kufyatua mato-fali.^f Waacheni wakajitafutie nyasi wenyewe. **8** Lakini bado mnapaswa kuwaamuru wafyatue idadi ileile ya mato-fali kama awali. Msiwapunguzie idadi, kwa sababu wanastarehe.* Ndiyo sababu wanalia, ‘Tunataka kwenda, tunataka kumtolea dhabihu Mungu wetu!’ **9** Watumikisheni zaidi, wapeni kazi zaidi ili wasisikilize uwongo.”

10 Basi wasimamizi wa kazi^g na wasimamizi wa watumwa wakaenda na kuwaambia watu: “Hivi ndivyo Farao anavyosema, ‘Siwapi tena nyasi.

5:4 *Au “mkabebe mizigo yenu.” 5:8 *Au “ni wavivu.”

11 Nendeni mkajitafutie nyasi zenu wenyewe popote mta- kapozipata, lakini kazi yenu haitapunguzwa hata kido- go.” 12 Ndipo watu wakata- wanyika kotekote katika nchi ya Misri ili kukusanya vishi- na vya mabua ili waweze ku- pata nyasi. 13 Na wasimami- zi wa kazi waliendelea kusisi- tiza hivi: “Ni lazima kila mmo- ja wenu amalize kazi yake kila siku, kama mlivyokuwa mki- fanya mlipokuwa mkiletewa nyasi.” 14 Pia, wasimamizi wa Waisraeli, ambao walikuwa wamechaguliwa na wasimami- zi wa kazi waliowekwa na Fa- rao kuwasimamia wasimami- zi hao wa Waisraeli, walipi- gwa.^a Waliwauliza: “Kwa nini hamkufyatua idadi ileile ya matofali mliyokuwa mkifya- tua mwanzoni? Hamkufanya hivyo jana na leo.”

15 Ndipo wasimamizi wa Waisraeli wakaenda kumlala- mikia Farao, wakisema: “Kwa nini unatutendea hivi sisi wa- tumishi wako? 16 Sisi watu- mishi wako hatupewi nyasi zozote, lakini wanatambia, ‘Fyatueni matofali!’ Tunapi- gwa, lakini kosa ni la watu wako.” 17 Lakini Farao aka- waambia: “Mnastarehe,^{*} mna- starehe!^{#b} Ndiyo sababu mna- sema, ‘Tunataka kwenda, tu- nataka kumtolea Yehova dha- bihu.’^c 18 Basi sasa, rudini kazini! Hamtapewa nyasi zo- zote, lakini ni lazima mfyatue idadi ileile ya matofali.”

19 Kwa hiyo wasimamizi wa Waisraeli wakatambua kwa- mba wako katika shida ku- bwa kwa sababu ya amri hii:

5:17 *Au “Ninyi ni wavivu.” #Au “ninyi ni wavivu.”

SURA YA 5

a Kut 2:11

b Kut 5:7, 8

c Kut 5:3

Safu ya 2

a Kut 6:9

b Kut 5:1

c Kut 5:6, 9

d Kut 3:8

SURA YA 6

e Kut 14:13

f Kut 9:3
Kut 11:1
Kut 12:29, 31g Mwa 17:1
Mwa 35:10, 11h Zb 83:18
Lu 11:2
Yoh 12:28
Mdo 15:14
Ufu 15:3i Mwa 12:8
Mwa 28:16
Yer 32:20j Mwa 15:18
Mwa 28:4

“Mspunguze hata kidogo ida- di ya matofali mnyapaswa kufyatua kila siku.” 20 Wa- lipotoka kwa Farao walikuta- na na Musa na Haruni, wa- liokuwa wamesimama waki- wangojea. 21 Mara moja wa- simamizi hao wakawaambia: “Yehova na awatazame ninyi na kuwahukumu, kwa maa- na mmefanya Farao na watu- mishi wake watudharau^{*} na- nyi mmeweka upanga mkono- ni mwao ili watuue.”^a 22 Ki- sha Musa akamgeukia Yehova na kumuuliza: “Yehova, kwa nini umewatesa watu hawa? Kwa nini umenituma? 23 Ta- ngu nilipofika mbele ya Farao kuzungumza katika jina lako,^b amewatesa vikali zaidi watu hawa,^c nawe hakika hujawao- koa watu wako.”^d

6 Basi Yehova akamwa- mbia Musa: “Sasa utaona mambo nitakayomtendea Fa- rao.^e Mkono wenye nguvu uta- mlazimisha awaruhusu watu wangu waende zao, na mkono wenye nguvu utamlazimisha awafukuze kutoka katika nchi yake.”^f

2 Kisha Mungu akamwa- mbia Musa: “Mimi ni Yehova. 3 Nami nilikuwa nikimto- kea Abrahamu, Isaka, na Ya- kobo kama Mungu Mweza- Yote,^g lakini kwa jina lan- gu Yehova^h sikujitambulisha kwao.ⁱ 4 Pia, nilifanya aga- no pamoja nao kwamba nita- wapa nchi ya Kanaani, nchi ambamo waliishi kama wageni.^j 5 Sasa mimi mwenyewe nimesikia kilio cha uchungu cha Waisraeli, ambao Wamisri

5:21 *Au “mmefanya tunuke uvundo mbele ya Farao na watumishi wake.”

wanawatumikisha kama watu-mwa, nami ninakumbuka agano langu.^a

6 "Kwa hiyo, waambie Waisraeli: 'Mimi ni Yehova, nami nitawatoa kutoka chini ya mizigo ya Wamisri na kuwaokoa kutoka katika utumwa wao,^b nami nitawakomboa kwa mkonono ulionyoo^{*} kwa hukumu kubwa.^c **7** Nami nitawachukua muwe watu wangu, nami nitakuwa Mungu wenu,^d nanyi hakika mtajua kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu anayewatoa kutoka chini ya mizigo ya Misri. **8** Nami nitawapeleka katika nchi niliyoapa^{*} kwamba nitampa Abrahamu, Isaka, na Yakobo; nitawapa ninyi iwe miliki yenu.^e Mimi ni Yehova."^f

9 Baadaye Musa akawapa Waisraeli ujumbe huo, lakini hawakumsikiliza Musa kwa sababu walikuwa wamevunjika moyo na kwa sababu ya utumwa wa kikatili.^g

10 Kisha Yehova akamwambia Musa: **11** "Nenda ukamwambie Farao, mfalme wa Misri, kwamba anapaswa kuwaruhusu Waisraeli waondoke katika nchi yake." **12** Lakini Musa akamwambia Yehova: "Tazama! Waisraeli hawajanisikiliza,^h Farao atanisikiliza-je mimi, mtu asiye na ufasha-ha?"ⁱ **13** Lakini Yehova akawaambia tena Musa na Haruni amri wanazopaswa kuwapa Waisraeli na pia Farao, mfalme wa Misri, ili kuwatoa Waisraeli katika nchi ya Misri.

14 Hawa ndio viongozi wa nyumba ya baba zao: Wana wa Rubeni, mzaliwa wa kwanza

SURA YA 6

a Mwa 17:1,7
Kut 2:24

b Kum 4:20

c Kum 26:8
1Nya 17:21
Mdo 13:17

d Kut 29:45
Kum 7:6
2Sa 7:24
Zb 33:12

e Mwa 15:18
Mwa 26:3
Mwa 35:12
Kut 32:13

f Kut 20:2
Isa 42:8

g Kut 5:21

h Kut 5:21
Kut 6:9

i Kut 4:10
Mdo 7:22

Safu ya 2

a Mwa 49:3

b Mwa 46:9

c 1Nya 4:24

d Mwa 29:34

e Mwa 46:11
Hes 26:57

f Hes 3:18

g Hes 3:19

h Hes 3:20

i Kut 2:1
Hes 26:59

j 1Nya 23:13

k Hes 16:1,32
Hes 26:10

l Law 10:4
Hes 3:30

m Ru 4:19-21
Mt 1:4

n Hes 3:2

o Hes 26:10,11

p Kut 26:58
1Nya 9:19

q Hes 3:32

r Hes 25:7
Hes 31:6
Yos 22:31
Amu 20:28

wa Israeli,^a walikuwa Hanoi, Palu, Hezroni, na Karmi.^b Hizo ndizo koo za Rubeni.

15 Wana wa Simeoni walikuwa Yemueli, Yamini, Ohadi, Yakini, Zohari, na Shauli, mwana wa mwanamke Mka-naani.^c Hizo ndizo koo za Simeoni.

16 Haya ndiyo majina ya wana wa Lawi,^d kulingana na koo zao: Gershoni, Kohathi, na Merari.^e Lawi aliishi miaka 137.

17 Wana wa Gershoni walikuwa Libni na Shimei, kulingana na koo zao.^f

18 Wana wa Kohathi walikuwa Amramu, Ishari, Hebroni, na Uzieli.^g Kohathi aliishi miaka 133.

19 Wana wa Merari walikuwa Mali na Mushi.

Hizo ndizo zilizokuwa koo za Walawi, kulingana na nasa-ba ya koo zao.^h

20 Sasa Amramu alimwoa Yokebedi, dada ya baba yake.ⁱ Akamzalia Amramu wana hawa: Haruni na Musa.^j Amramu aliishi miaka 137.

21 Wana wa Ishari walikuwa Kora,^k Nefegi, na Zikri.

22 Wana wa Uzieli walikuwa Mishaeli, Elsafari,^l na Sithri.

23 Sasa Haruni alimwoa Elisheba, binti ya Aminadabu, dada ya Nashoni.^m Akamzalia Haruni wana hawa: Nadabu, Abihu, Eleazari, na Ithamari.ⁿ

24 Wana wa Kora walikuwa Asiri, Elkana, na Abiasafu.^o Hizo ndizo zilizokuwa koo za Wakora.^p

25 Eleazari,^q mwana wa Haruni, alimwoa mmoja wa mabinti wa Putieli. Akamzalia mwana aliyeitwa Finehasi.^r

6:6 *Au "wenye nguvu." 6:8 *Tnn., "niliyooina mkono wangu." 6:12 *Tnn., "mtu ambaye hajatahiriwa midomo?"

Hao ndio viongozi wa koo* za Walawi, kulingana na koo zao.^a

26 Hao ndio Haruni na Musa walioambiwa na Yehova: "Watoeni Waisraeli katika nchi ya Misri, kundi kwa kundi."^b **27** Hao ndio waliozungumza na Farao, mfalme wa Misri, ili awaruhusu Waisraeli watoke Misri. Ilikuwa huyu Musa na Haruni.^c

28 Siku hiyo ambayo Yehova alizungumza na Musa katika nchi ya Misri, **29** Yehova alimwambia Musa: "Mimi ni Yehova. Mwambie Farao, mfalme wa Misri, kila jambo ninalokwambia." **30** Kisha Musa akamwambia Yehova: "Tazama! sina ufasaha,* sasa Farao atanisikilizaje?"^d

7 Kisha Yehova akamwambia Musa: "Tazama, nimekufanya kuwa kama Mungu* kwa Farao, na Haruni ndugu yako atakuwa nabii wako.^e **2** Unapaswa kurudia kila jambo nitakalokuamuru, na Haruni ndugu yako atazungumza na Farao, naye Farao atawaruhusu Waisraeli watoke katika nchi yake. **3** Lakini mimi, nitauacha moyo wa Farao uwe mkaidi,^f nami nita-zidisha ishara zangu na miujiza yangu katika nchi ya Misri.^g **4** Lakini Farao hatawasikiliza ninyi, nami nitauweka mkono wangu juu ya Misri na kuyatoa makundi yangu makubwa,* watu wangu, Waisraeli, kutoka katika nchi ya Misri kwa hukumu kubwa.^h **5** Na Wamisri watajua kwa hakika

6:25 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 6:26 *Tnn., "kulingana na majeshi yao." 6:30 *Tnn., "sijatahiriwa midomo." 7:1 *Tnn., "nimekufanya Mungu." 7:4 *Tnn., "majeshi yangu."

SURA YA 6

a Kut 6:19

b Kut 7:2, 4
Kut 12:41
Mdo 7:35

c Zb 77:20

d Kut 4:10
Kut 6:12

SURA YA 7

e Kut 4:14-16
Kut 4:30f Kut 4:21
Kut 7:13, 22
Kut 8:15, 19
Kut 9:12, 35
Kut 10:20, 27
Kut 11:10
Kut 14:8
Ro 9:17, 18g Kut 3:19, 20
Zb 105:26, 27
Mdo 7:36

h Kut 12:12, 51

Safu ya 2

a Kut 7:17
Kut 8:9, 10
Kut 8:22
Kut 9:29
Kut 14:4b Kum 34:7
Mdo 7:22, 23

c Kut 4:2, 3

d Mwa 41:8
ZTi 3:8e Kut 7:20, 22
Kut 8:7, 18
Kut 9:11

f Kut 7:3

g Kut 10:1

kwamba mimi ni Yehova^a nitakapounyoosha mkono wangu dhidi ya Misri na kuwatoa Waisraeli miongoni mwao." **6** Musa na Haruni wakafanya mambo ambayo Yehova aliwaamuru; hivyo ndivyo walivyofanya. **7** Musa alikuwa na umri wa miaka 80 naye Haruni alikuwa na umri wa miaka 83 walipozungumza na Farao.^b

8 Sasa Yehova akamwambia Musa na Haruni: **9** "Farao akiwaambia, 'Fanyeni muujiza,' mwambie Haruni, 'Chukua fimbo yako uitupe chini mbele ya Farao.' Itakuwa nyoka mkubwa."^c **10** Basi Musa na Haruni wakaenda kwa Farao na kufanya kama tu Yehova alivyokuwa amewaaamuru. Haruni akaitupa chini fimbo yake mbele ya Farao na watumishi wake, nayo ikawa nyoka mkubwa. **11** Hata hivyo, Farao akawaita watu wenye hekima na walozi, na makuhani wachawi wa Misri^d nao pia wakafanya muujiza huohuo kwa uchawi wao.^e **12** Kila mmoja wao akatupa chini fimbo yake, nazo zikawa nyoka wakubwa; lakini fimbo ya Haruni ikazimeza fimbo zao. **13** Lakini moyo wa Farao uliendelea kuwa mkaidi,^f na kama Yehova alivyosema, Farao hakuwasikiliza.

14 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Moyo wa Farao ni mgumu.^g Amekataa kuwaruhusu watu wangu waenda zao. **15** Nenda kwa Farao asubuhi. Tazama! Anaenda mtoni! Unapaswa kusimama kwenye ukingo wa Mto Nile; na ubebe mkononi ile fimbo iliyogeuka

7:11 *Au "ufundi wao wa uchawi."

kuwa nyoka.^a **16** Nawe unapaswa kumwambia, ‘Yehova Mungu wa Waebrania amenituma kwako,^b naye anasema: “Waruhusu watu wangu waende ili wanitumikie nyikani,” lakini mpaka sasa hujatii. **17** Yehova anasema hivi: “Kwa jambo hili utajua kwamba mimi ni Yehova.^c Tazama ninayapiga maji ya Mto Nile kwa fimbo hii iliyo mkononi mwangu, nayo yatabadilika na kuwa damu. **18** Samaki walio katika Mto Nile watakufa, nao Mto Nile utanuka, na Wamisri watashindwa kunywa maji ya Mto Nile.””

19 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Mwambie Haruni, ‘Ichukue fimbo yako na uunyooshe mkono wako juu ya maji yote ya Misri,^d juu ya mito yake, juu ya mifereji yake,* juu ya maeneo yake yenye umajimaji,^e na juu ya mabwawa yake yote, ili yawe damu.’ Kutakuwa na damu katika nchi yote ya Misri, hata katika vyombo vya mbaao na vya mawe.” **20** Mara moja Musa na Haruni wakafanya kama Yehova alivyowaa-muru. Akaiinua fimbo hiyo na kuyapiga maji ya Mto Nile mbele ya Farao na watumishi wake, na maji yote yaliyokuwa katika Mto Nile yakabadilika na kuwa damu.^f **21** Basi samaki waliokuwa mtoni wakafa,^g na mto ukaanza kunuka, na Wamisri hawakuweza kunywa maji ya Mto Nile,^h kulikuwa na damu katika nchi yote ya Misri.

22 Lakini makuhani wachawi wa Misri wakafanya jambo hilihilo kwa mazingaombwe

7:19 *Yaani, mifereji ya Mto Nile.

SURA YA 7

a Kut 4:2, 3

b Kut 3:18

c Kut 7:5
Kut 8:9, 10
Kut 8:22
Kut 9:29
Kut 14:4

d Kut 9:22
Kut 10:12
Kut 14:21

e Kut 8:5

f Zb 78:44

g Zb 105:29

h Kut 7:18, 24

Safu ya 2

a Kut 7:11, 12
Kut 8:7, 18
Kut 9:11
2Ti 3:8

b Kut 3:19

SURA YA 8

c Kut 3:12

d Zb 78:45

e Zb 105:30

yao,^a hivi kwamba moyo wa Farao ukaendelea kuwa mkaidi, na kama Yehova alivyo-sema, Farao hakuwasikiliza.^b **23** Basi Farao akarudi nyumbani kwake, wala hakuzingatia jambo hilo moyoni mwake. **24** Kwa hiyo, Wamisri wote walikuwa wakichimba kandokando kuzunguka Mto Nile wakitafuta maji ya kunywa, kwa sababu hawangeweza kunywa maji yoyote ya Mto Nile. **25** Na siku saba kamili zikapita baada ya Yehova kuupiga Mto Nile.

8 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Nenda kwa Farao umwambie, ‘Yehova anasema hivi: “Waruhusu watu wangu waende wakanitumikie.^c **2** Ukiendelea kukataa kuwaruhusu waondoke, nitaleta pigo la vyura katika eneo lako lote.^d **3** Nao Mto Nile utajaa vyura, nao watotoka humo na kuingia ndani ya nyumba yako, ndani ya chumba chako cha kulala, kitandani mwako, katika nyumba za watumishi wako na juu ya watu wako, ndani ya majiko yenu, na ndani ya vyombo vyenu vya* kukandia unga.^e **4** Vyura watapanda juu yako, juu ya watu wako, na juu ya watumishi wako wote.””

5 Baadaye Yehova akamwambia Musa: “Mwambie Haruni, ‘Unyooshe mkono wako ulio na fimbo juu ya mito, mifereji ya Nile, na maeneo yenye umajimaji, ili vyura waje juu ya nchi ya Misri.””

6 Basi Haruni akaunyoosha mkono wake juu ya maji ya Misri, na vyura wakaanza kuja na kuifunika nchi ya Misri.

8:3 *Au “mabakuli yenu ya.”

7 Hata hivyo, makuhani wachawi wakafanya jambo hilo-hilo kwa mazingaombwe yao, nao pia wakafanya vyura waje juu ya nchi ya Misri.^a 8 Ndi-po Farao akawaita Musa na Haruni na kuwambia: “Msihi-ni Yehova aniondolee mimi na watu wangu vyura hawa,^b kwa maana ninataka kuwaruhusu watu waende zao wakamoto-lee Yehova dhabihu.” 9 Ki-sha Musa akamwambia Farao: “Kwa heshima yako niambie wakati unaotaka nimwombe Mungu awaondoe vyura kuto-ka kwako, kutoka kwa watu-mishi wako, kutoka kwa watu wako, na kutoka katika nyum-ba zenu. Watabaki katika Mto Nile tu.” 10 Farao aka-mwambia: “Kesho.” Basi Musa akasema: “Itakuwa kama una-vyosema, ili ujue kwamba ha-kuna yeyote aliye kama Ye-hova Mungu wetu.^c 11 Vyura wataondoka kwako, kati-ka nyumba zako, kutoka kwa watumishi wako, na kutoka kwa watu wako. Watabaki ka-tika Mto Nile tu.”^d

12 Basi Musa na Haruni wa-kaondoka mbele ya Farao, naye Musa akamsihi Yehova amwondolee Farao vyura alio-mletea.^e 13 Kisha Yehova akafanya kama Musa ali-vyomwomba, na vyura wakaanza kufia nyumbani, nyuani, na mashambani. 14 Watu waka-kusanya marundo yasiyohesa-bika ya vyura, na nchi ikaa-nza kunuka. 15 Farao ali-poona kwamba hali ni nafuu, akaufanya moyo wake kuwa mgumu,^f na kama Yehova ali-vyosema, Farao akakataa ku-wasikiliza.

16 Sasa Yehova akamwa-mbia Musa: “Mwambie Haru-

SURA YA 8

a Kut 7:11, 12
Kut 7:20, 22
Kut 8:17, 18
Kut 9:11
2Ti 3:8

b Kut 10:16-19

c Kut 9:14
Kut 15:11
Zb 83:18
Zb 86:8
Isa 46:9
Yer 10:6, 7
Ro 9:17

d Kut 8:3

e Kut 8:30, 31
Kut 9:33

f Kut 4:21
Kut 7:3

Safu ya 2

a Zb 105:31

b Kut 7:11, 12
Kut 7:20, 22
Kut 8:7
Kut 9:11

c Kut 31:18
Lu 11:20

d Kut 9:4, 26
Kut 10:23
Kut 12:13

e 1Sa 17:46
1Fa 20:28
2Fa 19:17, 19

ni, ‘Inyooshe fimbo yako na uyapige mavumbi ya ardhi, nayo yatakuwa mbu* katika nchi yote ya Misri.’” 17 Nao wakafanya hivyo. Haruni akaunyoosha mkono wake uliokuwa na fimbo yake na ku-yapiga mavumbi ya ardhi, na mbu wakawavamia wanadamu na wanyama. Mavumbi yote katika nchi yote ya Misri yaka-wa mbu.^a 18 Makuhani wa-chawi wakajaribu pia kugeuza mavumbi yawe mbu kwa ma-zingaombwe yao,^b lakini ha-wakuweza. Mbu hao wakawa-vamia wanadamu na wanya-ma. 19 Basi makuhani wa-chawi wakamwambia Farao: “Ni kidole cha Mungu!”^c Laki-ni moyo wa Farao ukaendelea kuwa mkaidi, na kama Yehova alivyosema, hakuwasikiliza.

20 Kisha Yehova akamwa-mbia Musa: “Amka asubuhi na mapema ukasimame mbele ya Farao. Tazama! Ana-nda mtoni! Nawe unapaswa kumwambia, ‘Yehova anasema hivi: “Waruhusu watu wangu waende wakanitumi-kie. 21 Lakini usipowaruhusu watu wangu waende zao, nitakuletea nzi,* wewe, watumishi wako, na watu wako, nao wataingia katika nyumba zako; na nyumba za Misri zitajaa nzi hao, nao wataifu-nika hata ardhi ambayo Wa-misri wamesimama juu yake. 22 Siku hiyo, hakika nitaitenga nchi ya Gosheni, wa-nakoishi watu wangu. Haku-na nzi yeyote atakayepatika-na huko,^d na kwa jambo hilo utajua kwamba mimi, Ye-hova, niko humu nchini.^e

8:16 *Aina ya mbu anayeitwa *hak-kin-nam* katika Kiebrania. 8:21 *Aina ya nzi anayeuma.

23 Nami nitatofautisha kati ya watu wangu na watu wako. Kesho ishara hii itatokea.””

24 Basi Yehova akafanya kama alivyosema, na makundi makubwa sana ya nzi yakaaanza kuvamia nyumba ya Farao na nyumba za watumishi wake na nchi yote ya Misri.^a Nchi ikaharibiwa na nzi hao.^b

25 Hatimaye Farao akawaita Musa na Haruni na kuwambia: “Nendeni, mkamtolee dhahihu Mungu wenu nchini.”

26 Lakini Musa akasema: “Si vema kufanya hivyo, kwa sababu dhahihu tutakazomtolea Yehova Mungu wetu zitawachukiza Wamisri.^c Tukitoe dhahihu zinazowachukiza Wamisri mbele ya macho yao, je, hawatatupiga mawe? **27** Tutasafiri kwa siku tatu nyikani, na huko tutamtolea Yehova Mungu wetu dhahihu kama alivyotuambia.”^d

28 Basi Farao akasema: “Nitawaruhusu mwende mkamtolee Yehova Mungu wenu dhahihu nyikani. Ila tu, msiende mbali sana. Msihini Mungu kwa niaba yangu.”^e

29 Musa akasema: “Sasa ninaenda zangu, nami nitamsihi Yehova, na kesho nzi wataondoka kwako Farao, kwa watumishi wako, na kwa watu wako. Lakini wewe, Ee Farao, unapaswa kuacha kutuchezea* kwa kukataa kuturuhusu kwenda kumtolea Yehova dhahihu.”^f **30** Kisha Musa akaondoka mbele ya Farao na kumsihi Yehova.^g **31** Basi Yehova akafanya kama Musa alivyomsihi, na nzi wakaondoka kwa Farao, kwa watumishi wake, na kwa watu wake. Hakubaki hata nzi mmoja.

8:29 *Au “kutuhadaa.”

SURA YA 8

a Kut 8:3

b Zb 78:45
Zb 105:31

c Mwa 46:33, 34
Kut 10:25, 26

d Kut 3:18

e Kut 8:8
Kut 9:28

f Kut 8:15

g Kut 9:33

Safu ya 2

SURA YA 9

a Kut 5:1
Kut 8:1

b Kut 7:4

c Kut 9:15

d Kut 8:22
Kut 10:23
Kut 11:7
Kut 12:13

e Zb 78:48

f Kut 4:21

32 Hata hivyo, kwa mara nyingine tena Farao akaufanya moyo wake kuwa mgumu naye hakuwaruhusu Waisraeli waende zao.

9 Kwa hiyo Yehova akamwambia Musa: “Nenda kwa Farao umwambie, ‘Yehova Mungu wa Waebrania anasema hivi: “Waruhusu watu wangu waende wakanitumikie.”^a

2 Lakini ukikataa kuwaruhusu waende zao, na ukiendelea kuwazuia, **3** tazama! mkono wangu mimi Yehova^b utaipiga mifugo yenu iliyo shambani. Nitawaletea pigo kali sana farasi, punda, ngamia, ng’ombe, na makundi yenu.^c **4** Na hakika mimi Yehova nitaitofautisha mifugo ya Waisraeli na mifugo ya Wamisri, na haku na mnyama yeyote wa Waisraeli atakayekufa.””^d **5** Zaidi ya hayo, Yehova aliweka wakati hususa, akasema: “Kesho, mimi Yehova nitafanya jambo hilo katika nchi hii.”

6 Na kesho yake Yehova akafanya hivyo, kila aina ya mifugo ya Wamisri ikaanza kufa,^e lakini hakuna mnyama hata mmoja wa Waisraeli aliyekufa. **7** Farao alipouliza, aliambiwa kwamba hakuna mnyama hata mmoja wa Waisraeli aliyekufa. Hata hivyo, moyo wa Farao ukaendelea kuwa mgumu, naye hakuwaruhusu Waisraeli waende zao.^f

8 Kisha Yehova akawambia Musa na Haruni: “Jazeni masizi ya tanuru* kwenye mikono yenu miwili, Musa anapaswa kuyarusha hewani mbele ya Farao. **9** Nayoyatakuwa mavumbi laini juu ya nchi yote ya Misri, kisha

9:8 *Au “kalibu.”

yatakuwa majipu yenye usaha kwenye miili ya wanadamu na wanyama katika nchi yote ya Misri.”

10 Basi wakachukua masizi kutoka katika tanuru* na kusimama mbele ya Farao, naye Musa akayarusha hewani, nayo yakawa majipu yenye usaha yaliyotokea kwenye miili ya wanadamu na wanyama. **11** Makuhani wachawi hawakuweza kusimama mbele ya Musa kwa sababu ya majipu hayo, kwa maana makuhani wachawi na Wamisri wote walikuwa wamepatwa na majipu hayo.^a **12** Lakini Yehova akauacha moyo wa Farao uwe mkaidi, na kama Yehova alivyokuwa amemwambia Musa, Farao hakuwasikiliza.^b

13 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Amka asubuhi na mapema uende ukasimame mbele ya Farao, umwambie, ‘Yehova Mungu wa Waebra- nia amesema hivi: “Waruhusu watu wangu waende wakanitumikie. **14** Kwa maana sasa ninayaelekeza mapigo yangu yote niupige moyo wako, niwapige watumishi wako, na watu wako, ili ujue kwamba hakuna yeyote aliye kama mimi katika dunia yote.^c **15** Kwa maana kufikia sasa ningekuwa nimeunyoosha mkono wangu kwa nguvu na kukupiga wewe na watu wako kwa pigo kali sana, nawe ungekuwa umefutiliwa* mbali kutoka duniani. **16** Lakini nimekuacha uendelee kuishi kwa sababu hii hasa: ili nikuo- nyeshe nguvu zangu na ili jina langu litangazwe katika du-

9:10 *Au “kalibu.” 9:15 *Au “umefagiliwa.”

SURA YA 9

a Kut 7:11, 12
Kut 7:20, 22
Kut 8:7, 18
2Ti 3:8

b Kut 4:21
Kut 8:31, 32
Kut 14:17

c Kut 8:9, 10
2Sa 7:22
Zb 83:18

Safu ya 2

a Kut 14:17
Yos 2:9, 10
1Nya 16:24
Met 16:4
Isa 63:12
Ro 9:17

b Zb 78:47
Zb 105:32

c Kut 10:4, 5

nia yote.^a **17** Je, bado unate- nda kwa kiburi dhidi ya watu wangu kwa kukataa kuwaru- husu waende zao? **18** Taza- ma, kesho wakati kama huu, nitaleta mvua kubwa sana ya mawe ambayo haijawahi kuo- nekana katika nchi ya Misri tangu mwanzo wake mpaka sasa. **19** Kwa hiyo, waambie watu watoe mifugo yote na vitu vyenu vyote vilivyo shambani na kuvingiza ndani ya nyumba. Kila mwanadamu na mnyama ambaye atapati- kana shambani na ambaye ha- takuwa ameingizwa ndani ya nyumba atakufa mvua hiyo ya mawe itakapomnyeshea.””

20 Mtumishi yeyote wa Fa- rao aliyeogopa neno la Yeho- va aliwaingiza haraka watumi- shi wake na mifugo yake ndani ya nyumba, **21** lakini yeyote ambaye hakuzingatia moyoni mwake neno la Yehova aliwaa- cha watumishi wake na mifu- go yake shambani.

22 Sasa Yehova akamwa- mbia Musa: “Unyooshe mko- no wako kuelekea mbinguni, ili mvua ya mawe inyeshe juu ya nchi yote ya Misri,^b iwanye- shee wanadamu na wanyama na mimea yote ya shambani nchini Misri.”^c **23** Kwa hiyo Musa akainyoosha fimbo yake kuelekea mbinguni, na Yeho- va akaleta ngurumo na mvua ya mawe, na moto* ukashu- ka duniani, na Yehova aka- fanya mvua ya mawe ien- delee kunyesha juu ya nchi ya Misri. **24** Kulikuwa na mvua ya mawe, na moto ulikuwa ukiwakawaka katikati ya mvua hiyo. Mvua hiyo ili- kuwa kubwa sana; mvua kama

9:23 *Labda ni radi kubwa.

hiyo haikuwa imewahi kuonekana Misri tangu nchi hiyo iwe taifa.^a **25** Mvua hiyo ya mawe ilipiga kila kitu kilichokuwa shambani katika nchi yote ya Misri, kuanzia mwanaadamu mpaka mnyama, iliharibu kabisa mimea yote na kuvunjavunja miti yote ya shambani.^b **26** Ila tu mvua hiyo ya mawe haikunyeshwa katika nchi ya Gosheni, ambako Waisraeli waliishi.^c

27 Basi Farao akaamuru Musa na Haruni waitwe, akawaambia: "Wakati huu nimetenda dhambi. Yehova ni mwadilifu, lakini mimi na watu wangu tumekosea." **28** Msihini Yehova ili radi na mvua hii ya mawe kutoka kwa Mungu ikome. Kisha nitakuwa tayari kuwaruhusu mwende zenu, hamtakaa tena zaidi." **29** Kwa hiyo Musa akamwambia: "Mara tu nitakapoondoka jijini, nitainyoosha mikononyangu mbele za Yehova. Ngurumo itakoma na mvua ya mawe haitaendelea kunyeshwa, ili ujue kwamba dunia ni ya Yehova."^d **30** Lakini tayari ninajua kwamba hata nikifanyanya hivyo, wewe na watumishi wako hamtamwogopa Yehova Mungu."

31 Sasa mimea ya kitani na shayiri ilikuwa imeharibiwa kabisa na mvua, kwa sababu mimea ya shayiri ilikuwa na masuke na mimea ya kitani ilikuwa imechanua maua. **32** Lakini ngano na kusemethi* haikuwa imeharibiwa, kwa sababu haikuwa imekomaa." **33** Basi Musa akao-

9:32 *Aina fulani ya ngano ya hali ya chini iliyopandwa nchini Misri. ^aAu "majira yake yalichelewa."

SURA YA 9

a Kut 9:18

b Zb 105:33

c Kut 8:22
Kut 9:3, 4
Kut 10:23
Kut 11:7
Kut 12:13d Kut 7:5, 17
Kut 8:9, 10
Kut 8:22
Kut 14:4
Kum 10:14
Zb 24:1

Safu ya 2

a Kut 10:17-19

b Kut 4:21
Kut 8:13, 15

c Kut 7:4

SURA YA 10

d Kut 4:21
Kut 9:34e Kut 9:15, 16
Zb 78:12
Ro 9:17f Kut 13:3, 8
Kum 4:9
Kum 6:20-22
Zb 44:1

g Kut 9:17

h Kut 9:31, 32

ndoka jijini kutoka mbele ya Farao, akainyoosha mikono yake mbele za Yehova, ngurumo na mvua ya mawe zikakoma na mvua ikaacha kunyeshwa nchini.^a **34** Farao alipoona kwamba mvua ya mawe, na ngurumo zimekoma, akatenda dhambi tena na kufanya moyo wake uwe mgumu,^b yeye pamoja na watumishi wake. **35** Na moyo wa Farao ukaendelea kuwa mkaidi, na kama Yehova alivyokuwa amesema kupitia Musa, Farao hakuwaruhusu Waisraeli waendelea zao.^c

10 Kisha Yehova akamwambia Musa: "Nenda kwa Farao, kwa sababu nimeacha moyo wake na mioyo ya watumishi wake iwe migumu,^d ili nifanye ishara hizi zangu mbele yake,^e **2** na ili uwatungazie wanao na wajukuu wako jinsi nilivyoiadhibu vikali Misri na ishara nilizofanya miongoni mwenu;^f nanyi hakika mtajua kwamba mimi ni Yehova."

3 Basi Musa na Haruni waenda kwa Farao na kumwambia: "Yehova Mungu wa Waebrania amesema hivi: 'Utakataa mpaka lini kujinyenyekeza kwangu?'^g Waruhusu watu wangu waende wakanatumikie. **4** Kwa maana ukiendelea kukataa kuwaruhusu watu wangu waende zao, kesho nitaleta nzige ndani ya mipaka yenu. **5** Nao wataifunika ardhi yote, hivi kwamba hamtaweza kuiona ardhi. Watakula kabisa mimea ambayo haikuharibiwa na mvua ya mawe ambayo mlibaki nayo, nao watakuia miti yenu yote inayomea shambani.^h **6** Watajaa ndani

ya nyumba zako, nyumba za watumishi wako wote, na nyumba zote za Misri, kwa kadiri ambayo baba zenu na mababu zenu hawajawahi kamwe kuona tangu walipozaliwa katika nchi hii mpaka leo.”^a Kisha akageuka na kuondoka mbele ya Farao.

7 Ndipo watumishi wa Farao wakamwambia: “Mtu huyu ataendelea kututesa* mpaka lini? Waruhusu watu hawa waende zao wakamtumikie Yehova Mungu wao. Je, bado huoni kwamba Misri imeharibiwa?” **8** Kwa hiyo Musa na Haruni wakarudishwa kwa Farao, akawaambia: “Nendeni, mkamtumikie Yehova Mungu wenu. Lakini ni nani hasa watakaenda?” **9** Musa akamjibu: “Tutaenda na vijana wetu, wazee wetu, wana wetu, mabinti wetu, kondoo wetu, na ng’ombe wetu,^b kwa maana tutamfanyia Yehova she-rehe.”^c **10** Akawaambia: “Ikiwa nitawaruhusu ninyi na watoto wenu mwende, basi kwa kweli Yehova yuko pamoja nanyi!^d Ni wazi kwamba mnakusudia kutenda jambo fulani ovu. **11** Hapana! Ni wanaume wenu peke yao watakaenda kumtumikia Yehova, kwa sababu hilo ndilo mlilomba.” Basi wakafukuzwa kutoka mbele ya Farao.

12 Sasa Yehova akamwambia Musa: “Unyooshe mkono wako juu ya nchi ya Misri ili nzige waje juu ya nchi ya Misri na kula mimea yote nchini, kila kitu ambacho hakiharibiwa na mvua ya mawe.” **13** Mara moja Musa akainyoosha fimbo yake juu ya nchi ya

10:7 *Tnn., “kuwa mtego kwetu.”

SURA YA 10

a Kut 9:24

b Kut 10:25, 26

c Kut 3:18
Kut 5:1

d Kut 12:31, 32

Safu ya 2

a Zb 78:46

b Kut 10:5
Zb 105:34, 35

c Kut 8:30, 31

d Kut 7:3
Kut 11:10
Ro 9:17, 18

Misri, na Yehova akasababisha upepo wa mashariki uvume nchini mchana kutwa na usiku kucha. Asubuhi ilipofika, upepo huo wa mashariki ukaleta nzige. **14** Na nzige hao wakaja juu ya nchi yote ya Misri na kufunika eneo lote la Misri.^a Walikuwa wengi kupindukia;^b nzige wengi sana hivyo hawakuwa wamewahi kuonekana, wala nzige wengi sana hivyo hawangeonekana tena kamwe. **15** Waliifunika nchi yote, na nchi ikawa na giza kwa sababu yao; walitafuna mimea yote nchini na matunda yote mitini ambayo hayakuharibiwa na mvua ya mawe; hakuna majani yoyote yaliyobaki mitini wala kwenye mimea ya shambani katika nchi yote ya Misri.

16 Basi Farao akawaita haraka Musa na Haruni na kuwaambia: “Nimemtendea dhambi Yehova Mungu wenu na ninyi pia. **17** Sasa, tafadhali, mnisamehe dhambi yangu mara hii moja tu, na kumsihi Yehova Mungu wenu angalau aniondolee pigo hili hatari.” **18** Basi akaondoka* kwa Farao na kumsihi Yehova.^c **19** Kisha Yehova akasababisha upepo huo ubadili mkondo, nao ukawa upepo wenye nguvu sana wa magharibi, ukawapeperusha nzige hao na kuwapeleka katika Bahari Nyekundu. Hakuna nzige hata mmoja aliyebaki katika eneo lote la Misri. **20** Hata hivyo, Yehova aliuacha moyo wa Farao uwe mkaidi,^d naye hakuwaruhusu Waisraeli wae-nde zao.

10:18 *Inaelekea ni Musa.

21 Basi Yehova akamwambia Musa: “Unyooshe mkono wako kuelekea mbinguni ili giza liifunike nchi ya Misri, giza zito sana hivi kwamba linaweza kuguswa.” **22** Mara moja Musa akaunyoosha mkono wake kuelekea mbinguni, na giza zito sana likaifunika nchi yote ya Misri kwa siku tatu.^a **23** Hawakuonana, na kwa siku tatu hakuna yeyote kati yao aliyeondoka mahali alipokuwa; lakini Waisraeli wote walikuwa na mwanga za katika makao yao.^b **24** Kisha Farao akamwita Musa na kumwambia: “Nendeni, mkamtumikie Yehova.^c Ni kondoo wenu na ng’ombe wenu tu watakaobaki. Hata watoto wenu wanaweza kwenda nanyi.” **25** Lakini Musa akasema: “Wewe mwenyewe tupatie dhabihu na matoleo ya kuteketezwa, nasi tutazitoa kwa Yehova Mungu wetu.^d **26** Tutanda pia na mifugo yetu. Hatutamwacha mnyama yeyote,* kwa sababu tutawatoa dhabihu baadhi ya wanyama hao tunapomwabudu Yehova Mungu wetu, na hatujui ni mnyama gani tutakayemtoa Yehova kuwa dhabihu mpaka tutakapofika huko.” **27** Kwa hiyo Yehova akauacha moyo wa Farao uwe mkaidi, naye hakukubali kuwaruhusu waende zao.^e **28** Farao akamwambia: “Ondoka mbele yangu! Usithubutu kuuona uso wangu tena, kwa maana siku utakapouona uso wangu, utakufa.” **29** Ndipo Musa akasema: “Na iwe kama ulivyosema, sitathubutu kuuona uso wako tena.”

10:26 *Tnn., “Hatutaacha ukwato wote.”

SURA YA 10

a Zb 105:28

b Kut 8:21, 22
Kut 9:3, 6
Kut 9:26
Kut 11:7
Kut 12:13c Kut 8:28
Kut 9:28d Kut 3:18
Kut 5:3e Kut 4:21
Kut 14:4

Safu ya 2

SURA YA 11

a Kum 4:34

b Kut 12:31, 32

c Kut 3:21, 22
Kut 12:35, 36
Zb 105:37

d Kut 12:29

e Kut 4:22, 23
Zb 78:51
Zb 105:36
Zb 136:10
Ebr 11:28

f Kut 12:12

g Kut 12:30

h Kut 8:22
Kut 9:3, 4
Kut 10:23
Kut 12:13

i Kut 12:33

11 Ndipo Yehova akamwambia Musa: “Nitamletea Farao na Misri pigo moja zaidi. Baada ya pigo hilo atawaruhusu mwondoke hapa.^a Atakapowaruhusu mwondoke, atawafukuza kabisa kutoka hapa.^b **2** Sasa waambie watu kwamba wanaume wote na wanawake wote wanapasa kuwaomba majirani wao vito vya fedha na dhahabu.”^c **3** Basi Yehova akawafanya watu wapate kibali machoni pa Wamisri. Isitoshe, wakati huo Musa mwenyewe alikuwa mtu anayeheshimiwa sana na watumishi wa Farao na watu wengine nchini Misri.

4 Basi Musa akasema: “Yehova amesema hivi: ‘Karibu katikati ya usiku, nita-pita katikati ya Misri,^d **5** na kila mzaliwa wa kwanza katika nchi ya Misri atakufa,^e kuanzia mzaliwa wa kwanza wa Farao anayeketi kwenye kiti chake cha ufalme mpaka mzaliwa wa kwanza wa kijakazi anayesaga nafaka kwa jiwe la kusagia, na kila mzaliwa wa kwanza wa mifugo.^f **6** Katika nchi yote ya Misri, kutakuwa na kilio kikubwa ambacho hakijawahi kamwe kuonekana na wala hakitaonekana tena kamwe.^g **7** Lakini haku-na hata mbwa atakayewabwekea* Waisraeli, iwe ni wana-damu au mifugo yao, ili mjue kwamba mimi Yehova ninaweza kutofautisha kati ya Wamisri na Waisraeli.’^h **8** Na watumishi wako wote hakika watakuja mbele zangu na kuniinama, wakisema, ‘Nenda, wewe na watu wote wanaokufuata.’ⁱ Na baada ya hapo, nitaondo-

11:7 *Tnn., “atakayeunoa ulimi wake dhidi ya.”

ka.” Ndipo akatoka mbele ya Farao kwa hasira kali.

9 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Farao hatakusikiliza,^a ili miujiza yangu iongezeke katika nchi ya Misri.”^b

10 Musa na Haruni walifanya miujiza hiyo yote mbele ya Farao,^c lakini Yehova aliua-cha moyo wa Farao uwe mkaidi, hivi kwamba hakuwaruhusu Waisraeli waondoke katika nchi yake.^d

12 Sasa Yehova akawambia Musa na Haruni katika nchi ya Misri: **2** “Mwezi huu utakuwa kweni mwanzo wa miezi. Utakuwa mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu.^e **3** Liambieni kusanyiko lote la Waisraeli hivi: ‘Siku ya kumi ya mwezi huu, kila mmoja wao anapaswa kuchukua kondoo kwa ajili ya nyumba ya baba yake, kondoo^f mmoja kwa kila nyumba. **4** Lakini ikiwa familia ina watu wachache hivi kwamba hawawezi kummaliza kondoo mmoja, watagawana na jirani yao* wa karibu ndani ya nyumba yao kulingana na idadi ya watu.^g Mnapofanya hesabu, kadirieni kiasi cha nyama ya kondoo kitakacholiwa na kila mtu. **5** Kondoo wenu anapaswa kuwa kondoo dume wa mwaka mmoja, asiye na kasoro.^g Mnaweza kuchagua mwanakondoo dume au mwanambuzi. **6** Mtamtunza mpaka siku ya 14 ya mwezi huu,^h na familia zote katika kusanyiko la Israeli zinapaswa kumchinja jioni kabla ya giza kuingia.*ⁱ **7** Watachukua kiasi fulani cha damu na kuinyu-

12:4 *Tnn., “atagawana na jirani yake.”
12:6 *Tnn., “katikati ya zile jioni mbili.”

SURA YA 11

a Kut 3:19
 Kut 7:4
 Ro 9:17, 18

b Kut 7:3

c Zb 135:9

d Kut 4:21
 Kut 9:15, 16
 Kut 10:20

SURA YA 12

e Kut 13:4
 Kut 23:15
 Hes 28:16
 Kum 16:1

f Yoh 1:29
 1Ko 5:7
 Ufu 5:6

g Law 22:18-20
 Kum 17:1
 1Pe 1:19

h Hes 28:16

i Kut 12:18
 Law 23:5
 Kum 16:6

Safu ya 2

a 1Ko 5:7
 Ebr 11:28

b Kum 16:6, 7

c Kut 13:3
 Kut 34:25
 Kum 16:3
 1Ko 5:8

d Hes 9:11

e Law 7:15
 Law 22:29, 30
 Kum 16:4

f Kut 11:4, 5
 Kut 12:29

g Hes 33:4

h Kut 8:22
 Kut 9:4, 26
 Kut 10:23
 Kut 11:7

nyiza kwenye miimo miwili ya mlango na kwenye kizingiti cha juu cha mlango wa nyumba ambamo watamla mnyama huyo.^a

8 “Ni lazima waile nyama hiyo usiku huo.^b Wanapaswa kuichoma juu ya moto na kuila pamoja na mikate isiyo na chachu^c na mboga chungu za majani.^d **9** Msile sehemu yoyote ya nyama hiyo ikiwa mbichi au ikiwa imechemshwa, yaani, ikiwa imepikwa kwa maji, lakini ichomeni juu ya moto, kichwa chake pamoja na miguu yake na viungo vyake vya ndani. **10** Hampaswi kuhifadhi sehemu yoyote ya nyama hiyo mpaka asubuhi, lakini sehemu yoyote itakayobaki mpaka asubuhi mnapaswa kuitekeza kwa moto.^e **11** Na hivi ndivyo mnavyopaswa kuila, mkiwa mmejifunga mishipi,* mkiwa na viatu miguuni, na mkiwa na fimbo zenu mkononi; nanyi mnapaswa kuila haraka. Ni Pasaka ya Yehova. **12** Kwa maana nitapita katikati ya nchi ya Misri usiku huo na kumua kila mzaliwa wa kwanza katika nchi ya Misri, kuanzia mwanadamu mpaka mnyama;^f nami nitatekeleza hukumu dhidi ya miungu yote ya Misri.^g Mimi ni Yehova. **13** Ile damu itakuwa ishara inayoonyesha nyumba mta-kazokuwamo; nami nitaiona damu hiyo na kupita juu yenu, na pigo halitawajia na kuwangamiza ninyi nitakapoipiga nchi ya Misri.^h

14 “Siku hiyo itakuwa ukumbusho kwenu, nanyi mnapaswa kuisherehekea ikiwa

12:11 *Tnn., “mkiwa mmevifunga viuno vyenu.”

sherehe kwa Yehova katika vizazi vyenu vyote. Kwa kuwa ni sheria ya kudumu, mnapaswa kuisherehekea. **15** Kwa siku saba mtakula mikate isiyo na chachu.^a Naam, siku ya kwanza mtaondoa nyumbani mwenu unga uliokandwa wenye chachu, kwa sababu mtu yeyote atakayekula kitu kilichotiwa chachu kuanzia siku ya kwanza mpaka siku ya saba, ni lazima auawe kutoka katika Israeli. **16** Siku ya kwanza mtakuwa na kusanyiko takatifu, na siku ya saba, mtakuwa na kusanyiko lingine takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote siku hizo.^b Mtatarisha tu chakula kitakacholiwa na kila mtu.

17 “Mtaadhimisha Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu,^c kwa sababu siku hiyo, nitayatoa makundi yenu makubwa* katika nchi ya Misri. Nanyi mnapaswa kuiadhimisha siku hiyo katika vizazi vyenu vyote kwa kuwa ni sheria ya kudumu. **18** Katika mwezi wa kwanza, siku ya 14 ya mwezi huo, jioni, mnapaswa kula mikate isiyo na chachu mpaka siku ya 21 ya mwezi huo, jioni.^d **19** Kwa siku saba, unga uliokandwa ambao ume-tiwa chachu usipatikane ndani ya nyumba zenu, kwa sababu yeyote akila kitu kilichotiwa chachu, awe ni mgeni au mwenyeji wa nchi,^e mtu huyo lazima auawe kutoka katika kusanyiko la Israeli.^f **20** Hampaswi kula kitu chochote kilichotiwa chachu. Mtakula mikate isiyo na chachu katika nyumba zenu zote.”

21 Musa akawaita wazee wote wa Israeli^g bila kukawia

12:17 *Tnn., “majeshi yenu.”

SURA YA 12

a Kut 23:15
Law 23:6

b Law 23:8

c Law 23:6
Lu 22:1
1Ko 5:8

d Law 23:5, 6

e Hes 9:14

f Kum 16:3
1Ko 5:7

g Kut 3:16
Hes 11:16

Safu ya 2

a Ebr 11:28

b Kum 16:3

c Yos 5:10

d Kut 13:3, 8
Kum 6:6, 7

e Ebr 11:28

na kuwaambia: “Nendeni mkachague wanyama wachanga* kwa ajili ya kila moja ya familia zenu, nanyi mchinje dhahihu ya Pasaka. **22** Kisha mtachovya tita la majani ya hisopo katika damu iliyo ndani ya beseni na kupiga kizingiti cha juu cha mlango na miimo yake miwili kwa tita hilo lenye damu; na mtu yeyote kati yenu asitoke nje ya mlango wa nyumba yake mpaka asubuhi. **23** Kisha Yehova atakapopita ili kuwapiga Wamisri na kuiona damu kwenye kizingiti cha juu cha mlango na kwenye miimo yake miwili, kwa hakika Yehova atapita juu ya mlango wenu, naye hataruhusu pigo la kifo liingie* katika nyumba zenu.^a

24 “Mnapaswa kuadhimisha tukio hili kwa kuwa ni sheria ya kudumu kwenu na kwa wana wenu.^b **25** Nanyi mtakapolingia katika nchi ambayo Yehova atawapa kama alivyoahidi, mnapaswa kuadhimisha tukio hilo.^c **26** Na wana wenu watakapowauliza, ‘Mwadhimisho huu una maana gani kwenu?’^d **27** mnapaswa kuwaambia, ‘Tunamtotea Yehova dhahihu ya Pasaka, ambaye alipita juu ya nyumba za Waisraeli nchini Misri alipowapiga Wamisri, lakini akaacha nyumba zetu.’”

Kisha watu wakainama chini na kusujudu. **28** Basi Waisraeli wakaenda na kufanya kama Yehova alivyomwamuru Musa na Haruni.^e Hivyo ndiyo walivyofanya.

29 Ndipo katikati ya usiku, Yehova akamua kila mzali-

12:21 *Yaani, wanakondoo au wanambuzi. 12:23 *Tnn., “maangamizi yaiingie.”

wa wa kwanza nchini Misri,^a kuanzia mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi kwenye kiti chake cha ufalme mpaka mzaliwa wa kwanza wa mateka aliyekuwa gerezani,* na kila mzaliwa wa kwanza wa mnyama.^b **30** Farao akaamka usiku huo pamoja na watumishi wake wote na Wamisri wengine wote, na kulikuwa na kilio kikubwa sana miongoni mwa Wamisri, kwa sababu hapakuwa na nyumba hata moja ambayo haikuwa na mtu aliyekufa.^c **31** Mara moja Farao akamwita Musa na Haruni^d usiku na kuwaambia: “Amkeni! Ondokeni kati ya watu wangu, ninyi wawili na Waisraeli wengine. Nendeni mka mtumikie Yehova, kama mliyosema.^e **32** Chukueni pia kondoo wenu na ng’ombe wenu mwende zenu, kama mliyosema.^f Lakini mnapaswa kunibariki pia.”

33 Na Wamisri wakaanza kuwahimiza Waisraeli wao ndoke haraka^g nchini “kwa sababu,” kama walivyosema, “sisi ni kama watu ambao tayari wamekufa!”^h **34** Basi Waisraeli wakachukua unga wao uliokandwa ambao haukuwa umetiwa chachu, pamoja na vyombo vyao vya* kukanidia vikiwa vimefungwa katika nguo zao mabegani mwao. **35** Waisraeli walifanya kama Musa alivyokuwa amewaaambia, wakawaomba Wamisri vito vya fedha na vya dhahabu na pia mavazi.ⁱ **36** Yehova akawafanya Waisraeli wapate kibali machoni pa Wamisri, hivi kwamba wakawapa

12:29 *Tnn., “katika nyumba ya tangi la maji.” 12:34 *Au “mabakuli yao ya.”

SURA YA 12

a Hes 33:4
Zb 78:51
Zb 105:36

b Mwa 15:14
Kut 11:4, 5
Hes 3:13
Zb 135:8

c Kut 11:6

d Kut 10:28, 29

e Kut 3:19, 20
Kut 6:1
Kut 10:8-11
Zb 105:38

f Kut 10:26

g Kut 12:11

h Kut 10:7

i Mwa 15:14
Kut 3:21
Kut 11:2
Zb 105:37

Safu ya 2

a Kut 3:22

b Mwa 47:11
Kut 1:11

c Hes 33:5

d Mwa 12:1, 2
Mwa 15:1, 5
Mwa 46:2, 3
Kut 1:7
Hes 2:32

e Hes 11:4

f Kut 12:31

g Mwa 46:2, 3
Mwa 47:27
Mdo 13:17

h Gal 3:17

i Kum 16:1

j Law 22:10

k Mwa 17:12, 23

walichoomba, nao wakachukua mali za Wamisri.^a

37 Kisha Waisraeli wakao ndoka Ramesesi^b kwenda Sukothi,^c wanaume wapatao 600,000 walio tembea kwa mituu, bila kuhesabu watoto.^d **38** Pia, kundi kubwa lenye mchanganyiko wa watu^{*e} lilienda pamoja nao, na vilevile kondoo na ng’ombe, naam, mifugo wengi sana. **39** Wakaanza kuoka mikate ya mvingo isiyo na chachu kwa kutumia unga uliokandwa walio beba kutoka Misri. Haukuwa umetiwa chachu kwa sababu walifukuzwa ghafla kutoka Misri hivi kwamba hawakuwa wamejitayarishia chakula chochote.^f

40 Waisraeli walikuwa wameishi nchini Misri^g kwa miaka 430.^h **41** Mwishoni mwa miaka hiyo 430, siku hiyohiyoyo, makundi yote makubwa ya watu wa* Yehova yalitoka nchini Misri. **42** Wanapaswa kuadhimisha usiku huo kwa sababu Yehova aliwatoa nchini Misri. Watu wote wa Israeli katika vizazi vyao vyote wanapaswa kumheshimu Yehova kwa kuadhimisha usiku huo.ⁱ

43 Kisha Yehova akawaambia Musa na Haruni, “Hii ndiyo sheria ya Pasaka: Haku na mgeni anayepaswa kuila.^j **44** Lakini ikiwa mtu yeyote ana mtumwa wa kiume aliye nunuliwa kwa pesa, unapaswa kumtahiri.^k Ndipo mtumwa huyo atakaposhiriki kuila. **45** Mhamiaji na kibarua hawataila. **46** Italiwa ndani ya

12:38 *Yaani, kundi kubwa lenye mchanganyiko wa watu ambao hawakuwa Waisraeli, kutia ndani Wamisri. 12:41 *Tnn., “majeshi yote ya.”

nyumba moja. Hampaswi kutoa nyama yoyote nje ya nyumba, nanyi hampaswi kuvunja mfupa wowote wa mnyama wa Pasaka.^a **47** Kusanyiko lote la Israeli litasherehekea Pasaka. **48** Ikiwa mgeni anaishi pamoja nawe, naye anataka kusherehekea Pasaka ya Yehova, ni lazima kila mwanamume wa familia yake atahiriwe. Kisha anaweza kukaribia ili kuisherehekea, naye atakuwa kama mwenyeji wa nchi. Lakini mwanamume yeyote ambaye hajatahiriwa hapaswi kuila Pasaka.^b **49** Sheria ileile itafuatwa na mwenyeji na mgeni anayeishi miongoni mweni.”^c

50 Basi Waisraeli wote wakafanya kama Yehova alivyomwamuru Musa na Haruni. Hivyo ndivyo walivyofanya. **51** Siku hiyohiyo, Yehova aliwatoa Waisraeli pamoja na makundi yao makubwa* kutoka katika nchi ya Misri.

13 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Nitakasie* kila mzaliwa wa kwanza wa kiume wa Waisraeli. Mzaliwa wa kwanza wa kiume wa mwanadamu na mnyama ni wangu.”^d

3 Ndipo Musa akawaambia watu: “Kumbukeni siku hii mliyotoka Misri,^e kutoka katika nyumba ya utumwa, kwa sababu kwa mkono wenyewe nguvu Yehova aliwatoa katika nchi hii.^f Kwa hiyo hampaswi kula kitu chochote kilichotiwa chachu. **4** Mnatoa Misri siku ya leo, mwezi wa Abibu.”^g **5** Mnapaswa kuia-dhimisha siku hii katika mwe-

12:51 *Tnn., “majeshi yao.” 13:2 *Tnn., “Niwekee kando; Nitengee.” 13:4 *Angalia Nyongeza B15.

SURA YA 12

a Hes 9:12
Zb 34:19, 20
Yoh 19:33, 36

b Hes 9:14

c Law 24:22
Hes 15:16

SURA YA 13

d Hes 3:13
Hes 18:15
Kum 15:19
Lu 2:22, 23

e Kut 12:42
Kum 16:3

f Kum 4:34
Ne 9:10

g Kum 16:1

Safu ya 2

a Kut 3:8
Kut 34:11

b Mwa 15:18
Kut 6:5, 8

c Kut 3:17
Kum 8:7-9

d Kut 12:15
Kut 34:18

e Kut 23:15

f Kum 16:3

g Kut 12:26, 27

h Kut 12:14
Kum 11:18

i Kut 12:24, 25

j Mwa 15:18

k Kut 22:29
Kut 34:19, 20
Law 27:26
Hes 3:13
Lu 2:22, 23

zi huu, Yehova atakapowaleta katika nchi ya Wakanaani, Wahiti, Waamori, Wahivi, na Wayebusi,^a nchi aliyowaa pia mababu zenu kwamba atawapa ninyi,^b nchi inayotiririka maziwa na asali.^c **6** Kwa siku saba mtakula mikate isiyo na chachu,^d na katika siku ya saba, mtamfanyia Yehova sherehe. **7** Mikate isiyo na chachu inapaswa kuliwa kwa siku hizo saba;^e nanyi msipatikane na kitu chochote kilicho na chachu^f wala unga wowote uliokandwa uliotiwa chachu katika eneo lenu lote.* **8** Na siku hiyo unapaswa kumwambia mwanao, ‘Ni kwa sababu ya mambo ambayo Yehova alinitendea nilipotoka Misri.’^g **9** Nayo itakuwa ishara mkononi mwako na ukumbusho kwenye paji la uso wako,^h ili sheria ya Yehova iwe kinywani mwako, kwa sababu kwa mkono wenye nguvu Yehova alikuwa Misri. **10** Unapaswa kuishika sheria hii kwa wakati wake uliowekwa, mwaka baada ya mwaka.ⁱ

11 “Yehova atakapokuleta katika nchi ya Wakanaani, ambayo amekuapia wewe na mababu zako kwamba atakupaja,^j **12** ni lazima umtolee Yehova kila mzaliwa wa kwanza wa kiume,* na pia kila mnyama dume wa mifugo yako anayezaliwa kwanza. Wazaliwa hao wa kiume ni wa Yehova.^k **13** Kila mzaliwa wa kwanza wa punda utamkomboa kwa kondoo, na usipomkomboa, basi unapaswa kumvunja shingo. Nawe unapaswa kumko-

13:7 *Tnn., “katika mipaka yenu yote.” 13:9 *Tnn., “katikati ya macho yako.” 13:12 *Tnn., “kila kifunga mimba.”

mboa kila mzaliwa wa kwanza wa kiume kati ya wanao.^a

14 “Mwanao akikuuliza badaye, ‘Jambo hili linamaanisha nini?’ basi unapaswa kumwambia, ‘Kwa mkono wenye nguvu Yehova alitutoa Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa.^b **15** Farao alipokataa kwa ukaidi kuturuhusu tuondoke,^c Yehova alimua kila mzaliwa wa kwanza nchini Misri, kuanzia mzaliwa wa kwanza wa mwanadamu mpaka mzaliwa wa kwanza wa mnyama.^d Ndiyo sababu ninamtolea Yehova wazaliwa wote wa kwanza wa kiume* kuwa dhabihu, na kumkomboa kila mzaliwa wa kwanza kati ya wanangu.’ **16** Hiyo inapaswa kuwa ishara mkononi mwako na utepe kwenye paji la uso wako,^e kwa sababu kwa mkono wenye nguvu Yehova alitutoa Misri.”

17 Basi Farao alipowaruhusu Waisraeli waondoke, Mungu hakuwaongoza kufuata njia ipitayo katika nchi ya Wafilisti, ingawa ilikuwa fupi. Kwa maana Mungu alisema: “Watu hawa wakikabili vita huenda wakabadili mawazo yao na kurudi Misri.” **18** Kwa hiyo Mungu akawafanya wazunguke kupitia njia ya nyikani inayoelekea kwenye Bahari Nyekundu.^f Lakini Waisraeli waliondoka katika nchi ya Misri wakiwa wamejipanga kivita. **19** Pia Musa alibeba mifupa ya Yosefu, kwa sababu Yosefu alikuwa amewaapisha hivi wana wa Israeli: “Mungu hatakosa kamwe kuwakazia uangalifu, nanyi mnapaswa kuiondoa huku mifupa yangu

13:15 *Tnn., “kila kifungua mimba.”
13:16 *Tnn., “katikati ya macho yako.”

SURA YA 13

a Hes 18:15

b Kum 7:7, 8

c Kut 5:2

d Kut 12:29
Zb 78:51

e Kum 11:18

f Kut 14:2, 3
Hes 33:5

Safu ya 2

a Mwa 50:24, 25
Yos 24:32
Ebr 11:22

b Kut 14:19

c Hes 9:15
Zb 78:14d Zb 105:39
1Ko 10:1

SURA YA 14

e Kut 13:17, 18

f Kut 7:13
Ro 9:17, 18g Kut 9:15, 16
Kut 15:11
Kut 18:10, 11
Yos 2:9, 10h Kut 7:5
Kut 8:22

i Kut 12:33

j Kut 14:23

na kwenda nayo.”^a **20** Wa-kaondoka Sukothi na kupiga kambi Ethamu, ukingoni mwa nyika.

21 Sasa Yehova alikuwa akiwatangulia mchana katika nguzo ya wingu ili awaongoze njiani,^b na wakati wa usiku katika nguzo ya moto ili awape nuru, waweze kusafiri mchana na usiku.^c **22** Ile nguzo ya wingu haikuwa ikiondoka mbele ya watu wakati wa mchana, wala nguzo ya moto wakati wa usiku.^d

14 Sasa Yehova akamwambia Musa: **2** “Waa-mbie Waisraeli kwamba wanapaswa kurudi na kupiga kambi mbele ya Pihahirothi, kati ya Migdoli na bahari, mbele ya Baal-sefoni.^e Mtapiga kambi mbele yake kando ya bahari. **3** Kisha Farao atasema hivi kuhusu Waisraeli, ‘Wanatangatanga nchini kwa sababu wamechanganyikiwa. Wamepotea nyikani.’ **4** Nitauacha moyo wa Farao uwe mkaidi,^f naye atawafuatia, nami nita-jiipatia utukufu kupitia Farao na jeshi lake lote;^g na Wamisri watajua kwa hakika kwamba mimi ni Yehova.”^h Basi Waisraeli wakafanya hivyo.

5 Baadaye mfalme wa Misri akajulishwa kwamba Waisraeli wamekimbiba. Mara moja, Farao na watumishi wake wakabadili nia kuwahusu Waisraeli,ⁱ wakasema: “Kwa nini tulifanya hivyo na kuwaruhusu Waisraeli waondoke, wasiwe watumwa wetu?” **6** Kwa hiyo akatayarisha magari yake ya vita, akaenda pamoja na watu wake.^j **7** Akachukua magari 600 ya vita yaliyo bora na magari mengine yote ya vita nchini Misri, na kila gari

lilikuwa na mashujaa. **8** Kwa hiyo Yehova akauacha moyo wa Farao mfalme wa Misri uwe mkaidi, naye akawafuatia Waisraeli, ambao walikuwa wakienda zao kwa ujasiri.*^a

9 Wamisri wakawafuatia,^b na farasi wote wa magari ya vita ya Farao na askari wake wapanda farasi na jeshi lake lilikuwa likiwakaribia Waisraeli walipokuwa wamepiga kambi kando ya bahari, karibu na Pihahirothi, mbele ya Baal-sefoni.

10 Farao alipokaribia, Waisraeli waliinua macho yao na kuwaona Wamisri wakifafuatia. Waisraeli wakaogopa na kuanza kumlilia Yehova.^c **11** Wakamwambia Musa: “Je, ni kwa sababu hakuna makaburi huko Misri ndiyo sababu umetuleta hapa tufie nyikani?^d Ni jambo gani hili ulilotutenda kwa kutotoa Misri? **12** Je, hili silo jambo tulilokuambia nchini Misri tuliposema, ‘Achana nasi, ili tuwatumikie Wamisri’? Kwa maana ni afadhali kwetu kuwatumikia Wamisri kuliko kufia nyikani.”^e **13** Ndipo Musa akawaambia watu: “Msiogope.^f Simameni imara muone jinsi Yehova atakavyowao-koa leo.^g Kwa maana Wamisri mnaowaona leo, hamtao-ona tena kamwe.^h **14** Yehova mwenyewe atawapigania ninyi,ⁱ nanyi mtakaa kimya.”

15 Sasa Yehova akamwambia Musa: “Kwa nini unaendelea kunililia? Waambie Waisraeli wawunje kambi. **16** Nawe inua fimbo yako na kuonyoosha mkono wako juu ya bahari na kuigawanya, ili Waisraeli wapite kwe-

SURA YA 14

a Hes 33:3

b Kut 15:9

c Yos 24:6, 7
Ne 9:9d Kut 16:3
Kut 17:3
Hes 14:2-4
Zb 106:7e Kut 5:21
Kut 6:6, 9f Hes 14:9
Kum 20:3
2Nya 20:15, 17
Zb 27:1
Zb 46:1
Isa 41:10

g 2Nya 20:17

h Kut 14:30
Kut 15:5
Zb 136:15i Kum 1:30
Kum 20:4
2Nya 20:29

Safu ya 2

a Kut 9:15, 16

b Kut 14:4
Ro 9:17, 18c Mwa 48:16
Kut 32:34
Hes 20:16
Yud 9

d Kut 13:21

e Yos 24:6, 7

f Zb 105:39

g Kut 14:16
Mdo 7:36h Ne 9:10, 11
Zb 78:13
Zb 136:13
Isa 63:12i Yos 2:9, 10
Zb 66:6
Zb 106:9
Zb 114:3j 1Ko 10:1
Ebr 11:29

k Kut 15:8

l Kut 14:17

nye nchi kavu katikati ya bahari. **17** Nami ninaiacha moyo ya Wamisri iwe mikaidi, ili waingie humo wakiwafuatia; kwa hiyo nitajipatia utukufu kupitia Farao na jeshi lake lote, magari yake ya vita, na askari wake wapanda farasi.^a **18** Na Wamisri watajua kwa hakika kwamba mimi ni Yehova nitakapojipatia utukufu kupitia Farao, magari yake ya vita, na askari wake wapanda farasi.”^b

19 Ndipo malaika wa Mungu wa kweli^c aliyekuwa akitangulia kambi ya Waisraeli akaondoka na kurudi nyuma yao, nayo nguzo ya wingu iliyokuwa mbele yao ikarudi nyuma na kusimama nyuma yao.^d

20 Kwa hiyo ikaja kati ya kambi ya Wamisri na kambi ya Waisraeli.^e Upande mmoja, wingu hilo lilikuwa giza. Upande mwingine, uliangaza usiku.^f Hivyo, kambi ya Wamisri hai-kuikaribia kambi ya Waisraeli usiku kucha.

21 Sasa Musa akaonyoosha mkono wake juu ya bahari;^g naye Yehova akaisukuma bahari nyuma usiku kucha kwa upepo wenye nguvu wa mashariki, maji yakagawanyika,^h kukawa na nchi kavuⁱ katikati ya bahari. **22** Kwa hiyo Waisraeli wakapita kwenye nchi kavu katikati ya bahari,^j huku maji yakisimama kama ukuta upande wao wa kulia na wa kushoto.^k **23** Wamisri wakawafuatia; farasi wote wa Farao, magari yake ya vita, na askari wake wapanda farasi wakaanza kuwafuatia katikati ya bahari.^l **24** Wakati wa kesho la asubuhi,^m Ye-

14:24 *Yaani, kuanzia saa 8 hivi usiku hadi saa 12 asubuhi.

14:8 *Tnn., “kwa mkono ulioinuliwa.”

hova alitazama kambi ya Wamisri kutoka kwenye ile nguzo ya moto na wingu,^a naye akaivuruga kambi ya Wamisri. **25** Alikuwa akiyang'oa magurudumu ya magari yao ya vita hivi kwamba waliyaendesha kwa shida, na Wamisri walikuwa wakisema: "Na tuwakimbie Waisraeli tusiwakaribie kamwe, kwa sababu Yehova anawapigania dhidi ya Wamisri."^b

26 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Unyooshe mkono wako juu ya bahari ili maji yarudi na kuwafunika Wamisri, magari yao ya vita, na askari wao wapanda farasi." **27** Mara moja Musa akaunyoosha mkono wake juu ya bahari, na asubuhi ilipokuwa ikikaribia, bahari ikarudia hali yake ya kawaida. Wamisri walipokuwa wakiikimbia bahari, Yehova akawakung'uta Wamisri katikati ya bahari.^c **28** Maji yaliyokuwa yakirudi yalifunika magari ya vita na askari wapanda farasi na wanajeshi wote wa Farao waliokuwa wameingia baharini kuwafuatia.^d Hakuna hata mmoja wao aliyekoka.^e

29 Lakini Waisraeli walite-mbea kwenye nchi kavu katikati ya bahari,^f na maji yalisimama kama ukuta upande wao wa kulia na wa kushoto.^g **30** Kwa hiyo Yehova akawaoko Waisraeli siku hiyo kuto-ka mikononi mwa Wamisri,^h nao Waisraeli wakawaona Wamisri wakiwa wamekufa kwenye ufuu wa bahari. **31** Pia Waisraeli waliona nguvu nyingi ambazo* Yehova alidhihisha dhidi ya Wamisri, basi

14:31 *Tnn., "mkono wenye nguvu ambao."

SURA YA 14

a Kut 13:21

b Kut 14:4

c Kut 15:1,4

d Kut 15:5,10
Kum 11:3,4
Yos 24:6,7
Ne 9:10,11
Zb 78:53
Ebr 11:29e Kut 14:13
Zb 106:11
Zb 136:15

f Zb 77:19

g Kut 15:8

h Kum 4:20
Zb 106:8-11

Safu ya 2

a Kut 4:31
Kut 19:9
Zb 106:12

SURA YA 15

b Amu 5:1
2Sa 22:1
Ufu 15:3c Kut 9:16
Kut 18:10,11
Zb 106:11,12d Kut 15:21
Zb 136:15

e Isa 12:2

f 2Sa 22:47
Isa 25:1

g Kut 3:15

h Zb 83:18
Zb 148:13

i Zb 24:8

j Kut 6:3
Isa 42:8

k Kut 14:27

l Kut 14:6,7

m Ne 9:10,11

n Zb 60:5
Zb 89:13

o Isa 37:23

watu wakaanza kumwogopa Yehova na kuwa na imani katika Yehova na Musa mtumishi wake.^a

15 Wakati huo Musa na Waisraeli wakamwambia Yehova wimbo huu:^b

"Acheni nimwimbie Yehova, kwa maana amekwezwa sana.^c

Farasi na mpandaji wake amewavurumisha baharini.^d

2 Nguvu zangu na uwezo wangu ni Yah,* kwa maana amekuwa wokovu wangu.^e

Huyu ni Mungu wangu, nitamsifu;^f Mungu wa baba yangu,^g nitamkweza.^h

3 Yehova ni shujaa mwenye nguvu.ⁱ Yehova ndilo jina lake.^j

4 Ametupa baharini magari ya vita ya Farao na jeshi lake,^k

Na mashujaa wake bora kabisa wamezama katika Bahari Nyekundu.^l

5 Mawimbi makubwa yaliwafunika; wakazama vilindini kama jiwe.^m

6 Mkono wako wa kuume, Ee Yehova, una nguvu nyingi;ⁿ

Mkono wako wa kuume, Ee Yehova, unaweza kumvunjavunja adui.

7 Katika fahari yako kuu unaweza kuwaangusha chini wale wanaoinuka juu dhidi yako;^o

Unaituma hasira yako inayowaka, nayo inawala kama majani makavu.

8 Kwa pumzi moja kutoka katika mianzi ya pua

15:2 *"Yah" ni ufupisho wa jina Yehova.

- yako maji yalikusanyika pamoja;
Yalisimama tuli, yakazuia mafuriko;
Mawimbi makubwa yali-gandamana katikati ya bahari.
- 9** Adui alisema, 'Nitawafuatia! Nitawafikia!
Nitagawanya nyara mpaka nitakapotosheka!
Nitauchomoa upanga wangu! Mkono wangu utawatiisha!'^a
- 10** Ulipuliza bahari kwa pumzi yako, ikawafunika;^b
Walizama kama madini ya risasi katika maji makuu.
- 11** Ni nani kati ya miungu aliye kama wewe, Ee Yehova?^c
Ni nani aliye kama wewe, unayejidhihirisha mwenyewe kuwa mkuu katika utakatifu?^d
Wewe unayestahili kuogopwa kwa nyimbo za sifa, Wewe unayetenda mambo yanayostaajabisha.^e
- 12** Uliunyoosha mkono wako wa kuume, dunia ikawameza kabisa.^f
- 13** Kwa upendo wako mshikamanifu umewaongoza watu uliowakomboa;^g
Kwa nguvu zako utawangoza kwenye makao yako matakatifu.
- 14** Ni lazima mataifa yasikie;^h yatatetemeka;
Wakaaji wa Ufilisti wata-shikwa na maumivu makali.*
- 15** Wakati huo mashehe* wa Edomu wataogopa sana,

15:14 *Tnn., "uchungu wa kuzaa."
15:15 *Shehe alikuwa mkuu wa kabila.

SURA YA 15

a Kut 14:5, 9

b Kut 14:21, 28

c Kum 3:24
2Sa 7:22

d Isa 6:3

e Kut 11:9

f Zb 78:53
Ebr 11:29

g Zb 106:10

h Hes 14:13, 14

Safu ya 2

a Hes 22:1, 3

b Yos 2:9-11
Yos 5:1

c Kum 11:25

d 2Sa 7:23
Isa 43:1e Hes 20:14, 17
Hes 21:21, 22

f Zb 80:8

g Zb 10:16

h Kut 14:23

i Kut 14:28

j Kut 14:22

k Kut 9:16
Kut 18:11

Na watawala wenye nguvu* wa Moabu wata-tetemeka.^a

Wakaaji wote wa Kanaani wataavunjika moyo.^b

16 Watashikwa na woga na hofu.^c

Kwa sababu ya ukuu wa mkono wako watatulia kama jiwe

Mpaka watu wako wataka-popita, Ee Yehova,
Mpaka watu uliowatokeza^d watakapopita.^e

17 Utawaleta na kuwapanda kwenye mlima wa urithi wako,^f

Mahali pa kudumu ulipotayarisha pawe makao yako, Ee Yehova,

Mahali patakatifu, Ee Yehova, ambapo umepajenga imara kwa mikono yako.

18 Yehova atatawala akiwa mfalme milele na milele.^g

19 Farasi wa Farao na magari yake ya vita na askari wake wapanda farasi walipoingia baharini,^h

Ndipo Yehova alipoyarudisha maji ya bahari yaka-wafunika,ⁱ

Lakini Waisraeli walitembea kwenye nchi kavu katikati ya bahari."^j

20 Kisha nabii Miriamu, dada ya Haruni, akachukua tari, na wanawake wote wakamfuata wakiwa na matari yao wakicheza dansi. **21** Miriamu akaimba hivi akiwaitikia wanaume:

"Mwimbieni Yehova, kwa maana amekwezwa sana.^k

15:15 *Au "watawala wa mabavu."

Farasi na mpandaji wake amewavurumisha baharini.^a

22 Baadaye Musa akawaozoga Waisraeli kutoka katika Bahari Nyekundu, wakanda katika nyika ya Shuri na kusafiri kwa siku tatu nyikani, lakini hawakupata maji.

23 Wakafika Mara,^{*b} lakini hawakuweza kunywa maji ya Mara kwa sababu yalikuwa machungu. Ndiyo sababu alipaita mahali hapo Mara.

24 Basi watu wakaanza kumnung'unikia Musa,^c wakisema: "Tutakunywa nini?"

25 Musa akamlilia Yehova,^d naye Yehova akamwelekeza kwenye mti fulani. Alipoutupa ndani ya maji hayo, yakawa matamu.

Huko Mungu akawawekea sharti na msingi wa hukumu, sharti na huko Mungu akawajaribu.^e

26 Alisema: "Ikiwa mtaisikiliza kwa makini sauti yangu mimi, Yehova Mungu wenu na kufanya yaliyo sawa machoni pangu na kusikiliza kwa makini amri zangu na kushika masharti yangu yote,^f sitawaletea ugonjwa wowote ambao niliwaletka Wamisri,^g kwa sababu mimi, Yehova, ninawaponya."^h

27 Baada ya hapo wakafika Elimu, mahali palipokuwa na chemchemi 12 za maji na mitende 70. Kwa hiyo wakapiga kambi hapo kando ya maji.

16 Baada ya kutoka Elimu, hatimaye kusanyiko lote la Waisraeli likafika katika nyika ya Sini,ⁱ kati ya Elimu na Sinai, siku ya 15 ya mwezi wa pili baada ya kutoka katika nchi ya Misri.

15:23 *Maana yake "Uchungu."

SURA YA 15

a Kut 14:27, 28
Zb 106:11, 12

b Hes 33:8

c Kut 16:2, 3
Kut 17:3
1Ko 10:6, 10

d Kut 17:4

e Kut 16:4
Kum 8:2

f Kum 28:1

g Kum 7:12, 15

h Kut 23:25
Zb 103:3

SURA YA 16

i Hes 33:10, 11

Safu ya 2

a Kut 15:24
1Ko 10:6, 10

b Hes 11:4
Hes 14:2, 3

c Kut 17:3
Hes 16:13

d Zb 78:24, 25
Zb 105:40
Yoh 6:31, 32
Yoh 6:58
1Ko 10:1, 3

e Mt 6:11

f Kum 8:2

g Kut 35:2

h Kut 16:22

i Kut 6:7
Hes 16:28, 29

j Hes 21:7
1Sa 8:7

2 Kisha kusanyiko lote la Waisraeli likaanza kuwanung'unikia Musa na Haruni nyikani.^a **3** Waisraeli waliendelea kuwanung'unikia wakisema: "Laiti mkono wa Yehova ungetuua katika nchi ya Misri tulipokuwa tukiketi kando ya vyungu vya nyama,^b tulipokuwa tukila na kushiba mikate. Sasa mmetutoa huko na kutuleta katika nyika hii ili kuliua kusanyiko hili lote kwa njaa kali."^c

4 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Tazama, ninawanyeshea mkate kutoka mbinguni,^d na kila mtu anapaswa kwenda kukusanya kiasi kinachomtosha siku baada ya siku,^e ili niwajaribu nione kama watafuata sheria yangu au la.^f **5** Lakini siku ya sita^g wanapotayarisha kiasi wali-chokusanya, kinapaswa kuwa mara mbili ya kiasi wanachokusanya kila siku, siku nyinginezo."^h

6 Kwa hiyo Musa na Haruni wakawaambia Waisraeli wote: "Jioni mtajua kwa hakika kwamba Yehova ndiye aliyewatoa ninyi nchini Misri.ⁱ **7** Asubuhi mtauona utukufu wa Yehova, kwa sababu Yehova amesikia manung'uniko yenu dhidi yake. Sisi ni nani hivi kwamba mnung'unike dhidi yetu?"

8 Musa akaendelea kusema: "Yehova atakapowapa nyama ya kula jioni na mikate mtakayokula asubuhi na kushiba, mtajua kwamba Yehova amesikia manung'uniko yenu mnyonung'unika dhidi yake. Lakini sisi ni nani? Hamnung'uniki dhidi yetu, bali dhidi ya Yehova."^j

9 Kisha Musa akamwambia Haruni: "Liambie hivi

kusanyiko lote la Waisraeli, 'Karibieni mbele za Yehova, kwa maana amesikia manung'uniko yenu.'"^a **10** Mara tu Haruni alipomaliza kuzunguma na kusanyiko lote la Waisraeli, waligeuka na kutazama nyikani, na tazama! utukufu wa Yehova ukatokea katika lile wingu.^b

11 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **12** "Nimesikia manung'uniko ya Waisraeli.^c Waambie hivi: 'Jioni kabla ya giza kuingia* mtakula nyama, na asubuhi mtashiba mikate,^d nanyi mtajua kwa hakika kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu.'"^e

13 Basi jioni hiyo kware wakaja na kufunika kambi,^f na asubuhi utando wa umande ulizunguka kambi yote. **14** Utando huo wa umande ulipotoweka, kitu laini, kinachovunjikavunjika,^g kitu laini kama theluji, kilienea kwenye ardhi nyikani. **15** Waisraeli walipokiona, walianza kuulizana: "Ni nini hiki?" kwa maana hawakujua kili kuwa nini. Musa akawaambia: "Ni mkate ambao Yehova amewapa uwe chakula chenu."^h **16** Yehova ameamuru hivi: 'Kila mtu anapaswa kukusanya kiasi anachoweza kula. Kila mmoja wenu atachukua kiasi cha omeri moja*ⁱ kwa ajili ya kila mtu aliyekatika hema lake.'" **17** Waisraeli wakaanza kukusanya; baadhi yao walikusanya zaidi na wengine wakakusanya kidogo. **18** Walipopima kwa omeri, yule aliyekusanya zaidi hakuwa na ziada na yule aliye-

16:12 *Tnn., "Katikati ya zile jioni mbili." **16:16** *Karibu lita 2.2. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 16

a Kut 16:2
Hes 11:1

b Kut 13:21
Hes 16:19
Mt 17:5

c Hes 14:27

d Zb 105:40

e Kut 4:5
Kut 6:7

f Hes 11:31, 34
Zb 78:27-29

g Hes 11:7
Kum 8:3
Ne 9:15

h Hes 21:5
Kum 8:14, 16
Yos 5:11, 12
Yoh 6:31, 32
Yoh 6:58
1Ko 10:1, 3

i Kut 16:36

Safu ya 2

a 2Ko 8:15

b Mt 6:11, 34

c Kut 16:5

d Kut 20:8
Kut 31:15
Kut 35:2
Law 23:3

e Hes 11:7, 8

f Kut 20:9, 10
Kut 31:13
Kum 5:15

kusanya kidogo hakupungukiwa.^a Kila mmoja alikusanya kiasi alichoweza kula.

19 Kisha Musa akawaambia: "Hakuna yeyote anayapaswa kuubakiza mkate huo mpaka asubuhi."^b **20** Lakini hawakumsikiliza Musa. Baadhi yao walipoubakiza mpaka asubuhi, ulipata mabuu na kunuka, hivyo Musa akawa-kasirikia sana. **21** Waliuokota asubuhi baada ya asubuhi, kila mtu kulingana na kiasi alichoweza kula. Jua lilipokuwa kali, uliyeyuka.

22 Siku ya sita, waliokota kiasi mara mbili,^c vipimo viwili vya omeri kwa kila mtu. Kwa hiyo wakuu wote wa kusanyiko wakaja na kumwambia Musa jambo hilo. **23** Musa akawaambia: "Hivyo ndivyo alivyosema Yehova. Kesho kutakuwa na pumziko kamili,* sabato takatifu kwa Yehova.^d Okeni mnachohitaji kuoka, na chemsheni mnachohitaji kuchemsha;^e kisha chochote kitakachobaki mkihifadhi mpaka asubuhi." **24** Basi waki-hifadhi mpaka asubuhi, kama Musa alivyowaamuru, nacho hakikunuka wala kuwa na mabuu. **25** Kisha Musa akasema: "Kuleni chakula hicho leo, kwa sababu leo ni sabato kwa Yehova. Leo hamtakipata kwenye ardhi. **26** Mtakiokota kwa siku sita, lakini siku ya saba ni Sabato,^f hakitakuwepo." **27** Lakini baadhi ya watu walienda kukiokota siku ya saba, lakini hawakupata chochote.

28 Kwa hiyo Yehova akamwambia Musa: "Mtakataa kushika amri na sheria zangu

16:23 *Au "mwadhimisho wa sabato."

mpaka lini?^a **29** Zingatieni kwamba mimi, Yehova, nime-wapa Sabato.^b Ndiyo sababu katika siku ya sita ninawapa mkate wa siku mbili. Kila mtu anapaswa kukaa mahali alipo; hakuna yeyote anayepaswa kutoka kwake siku ya saba.” **30** Kwa hiyo watu wakaadhimisha Sabato* siku ya saba.^c

31 Watu wa nyumba ya Israeli waliuita mkate huo “mana.”* Ulikuwa mweupe kama mbege za mgiligilani, na ladha yake ilikuwa kama ya keki bapa zenye asali.^d **32** Kisha Musa akasema: “Yehova ameamuru hivi: ‘Jazeni mkate huo katika kipimo cha omeri ili uwe kitu kitakachohifadhiwa katika vizazi vyenu vyote,^e ili watoto wenu waone mkate niliowa-pa mle nyikani nilipokuwa ni-kiwatoa katika nchi ya Misri.” **33** Basi Musa akamwambia Haruni: “Chukua mtungi na kutia humo omeri moja ya mana, nawe uiweke mbele za Yehova ili iwe kitu kitakachohifadhiwa katika vizazi vyenu vyote.”^f **34** Haruni akafanya kama Yehova alivyomwamuru Musa, akaiweka mbele ya sanduku la Ushahidi*^g ili ihifadhiwe. **35** Waisraeli walikuwa mana kwa miaka 40,^h mpaka walipofika katika nchi ili-yokaliwa na watu.ⁱ Walikula mana mpaka walipofika mpakani mwa nchi ya Kanaani.^j **36** Sasa omeri ni sehemu ya kumi ya kipimo cha efa.*

16:30 *Au “wakapumzika.” **16:31** *Labda linatokana na neno la Kiebrania linalomaanisha “Ni nini hiki?” **16:34** *Vitu muhimu vilihifadhiwa katika sanduku hili. **16:36** *Efa ilikuwa sawa na lita 22 au kilogramu 13 hivi. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 16

a Hes 14:11
Zb 78:10
Zb 106:13

b Kut 31:13

c Law 23:3
Kum 5:13, 14

d Kut 16:15
Hes 11:7

e Zb 105:5, 40

f Ebr 9:4

g Kut 27:21

h Kum 8:2
Ne 9:21
Zb 78:24

i Yos 5:11, 12

j Hes 33:48
Kum 34:1

Safu ya 2

SURA YA 17

a Hes 33:12

b Hes 33:2

c Hes 33:14

d Kut 5:19, 21
Hes 14:2, 3
Hes 20:3

e Hes 14:22
Zb 78:18, 22
Zb 106:14

f Kut 16:2, 3

g Kut 7:20

h Hes 20:8
Kum 8:14, 15
Ne 9:15
Zb 78:15
Zb 105:41
1Ko 10:1, 4

i Kum 9:22

j Zb 81:7

k Kum 6:16
Zb 95:8, 9
Ebr 3:8, 9

l Mwa 36:12

17 Kusanyiko lote la Waisraeli likaondoka katika nyika ya Sini^a hatua kwa hatua kama Yehova alivyoagiza,^b wakapiga kambi Refidimu.^c Lakini watu hawakuwa na maji ya kunywa.

2 Basi watu wakaanza kugombana na Musa^d wakisema: “Tupe maji ya kunywa!” Lakini Musa akawauliza: “Kwa nini mnagombana nami? Kwa nini mnaendelea kumjaribu Yehova?”^e **3** Lakini watu walikuwa na kiu sana mahali hapo, nao wakaendelea kumnung’unikia Musa^f wakisema: “Kwa nini umetupandisha kutoka Misri ili kutuua kwa kiu sisi na wana wetu na kifugo yetu?”

4 Mwishowe Musa akamlilia Yehova akisema: “Nifanye nini na watu hawa? Hivi punde watanipiga mawe!”

5 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Nenda mbele ya watu, wachukue wazee kadhaa wa Israeli na fimbo yako uliyotumia kupiga maji ya Mto Nile.^g Ibebe mkononi mwako na uendelee kutembea. **6** Tazama! Nitakuwa nimesimama mbele yako kwenye mwamba huko Horebu. Unapaswa kuu-piga mwamba huo, na maji yatoka ndani yake, kisha watu watayanywa.”^h Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. **7** Basi akapaita mahali hapo Masa*ⁱ na Meriba,^{#j} kwa sababu ya ugomvi wa Waisraeli na kwa sababu wali-mjaribu^k Yehova kwa kusema: “Je, Yehova yuko katikati yetu au la?”

8 Kisha Waamaleki^l wakaja na kupigana na Waisraeli huko

17:7 *Maana yake “Kujaribu; Jaribu.”
#Maana yake “Kugombana.”

Refidimu.^a **9** Ndipo Musa akamwambia Yoshua:^b “Tuchagulie wanaume wakapigane na Waamaleki. Kesho nitasima juu ya kilima, nikiwa na fimbo ya Mungu wa kweli mkononi mwangu.” **10** Basi Yoshua akafanya kama Musa alivyomwambia,^c akapigana na Waamaleki. Naye Musa, Haruni, na Huru^d wakapanda juu ya kilima.

11 Wakati wote ambapo Musa aliinua mikono yake, Waisraeli walishinda, lakini mara tu alipoishusha mikono yake, Waamaleki walishinda. **12** Mikono ya Musa ilipochoka, walichukua jiwe wakaliweka chini yake, akaketi juu ya jiwe hilo. Kisha Haruni na Huru, mmoja upande huu na mwingine upande mwingine, wakaitegemeza mikono yake, hivi kwamba mikono yake ikabaki imara mpaka jua lilipotua. **13** Kwa hiyo Yoshua akawashinda kwa upanga Waamaleki na watu walio-shirikiana nao.^e

14 Sasa Yehova akamwambia Musa: “Andika jambo hili katika kitabu liwe ukumbusho,* na uliseme tena kwa Yoshua: ‘Nitawaangamiza kabisa Waamaleki kutoka chini ya mbingu, nao hawatakumbukwa tena.’”^f **15** Kisha Musa akajenga madhabahu na kuilita Yehova-nisi,* **16** na kusema: “Kwa sababu mkono wa Waamaleki unapinga kiti cha ufalme cha Yah,^g Yehova atapigana vita na Waamaleki kizazi baada ya kizazi.”^h

17:14 *Au “kikumbusho.” 17:15 *Maana yake “Yehova Ni Nguzo Yangu ya Ishara.”

SURA YA 17

a Kum 25:17
1Sa 15:2

b Hes 11:28

c Yos 11:15

d Kut 24:13, 14

e Yos 11:12

f Hes 24:20
Kum 25:19
1Nya 4:42, 43

g Ufu 19:1

h 1Sa 15:20
Est 9:24

Safu ya 2

SURA YA 18

a Kut 2:16, 21
Kut 3:1

b Yos 2:9, 10
Yos 9:3, 9

c Mdo 7:29

d Kut 2:22

e Kut 2:15

f Kut 19:2
1Fa 19:8, 9

g Kut 4:18
Hes 10:29

h Kut 7:3
Kut 14:27, 28
Kum 4:34

i Kut 15:22
Kut 16:3

18 Sasa Yethro kuhani wa Midiani, baba mkwe wa Musa,^a akasikia mambo yote ambayo Mungu alikuwa amemtendea Musa na watu wake Waisraeli, jinsi Yehova alivyowatoa Waisraeli nchini Misri.^b **2** Yethro, baba mkwe wa Musa, alikuwa amemchukua Sipora mke wa Musa ili amtunze, Sipora aliporudishwa **3** pamoja na wanawe wawili.^c Mwana mmoja aliitwa Gershomo,^{*d} kwa sababu Musa alisema, “Nimekuwa mkaaaji mgeni katika nchi ya kigeni,” **4** na yule mwingine aliitwa Eliezeri,^{*e} kwa sababu Musa alisema, “Mungu wa baba yangu ni msaidizi wangu, aliyeniokoa kutokana na upanga wa Farao.”^e

5 Basi Yethro, baba mkwe wa Musa, pamoja na wana mke wa Musa, wakaja kwa Musa nyikani ambako alikuwa amepiga kambi karibu na mlima wa Mungu wa kweli.^f **6** Kisha akatuma ujumbe huu kwa Musa: “Mimi, Yethro, baba mkwe wako,^g naja kwako pamoja na mke wako na wanawe wawili.” **7** Mara moja Musa akaenda kumpokea baba mkwe wake, akainama chini na kumbusu. Wakajuliana hali, kisha wakaingia hemani.

8 Musa akamsimulia baba mkwe wake mambo yote ambayo Yehova alikuwa amemtendea Farao na Wamisri kwa ajili ya Waisraeli,^h matazizo yote waliyopata safarini,ⁱ na jinsi Yehova alivyowaokoa. **9** Yethro akashangilia kwa sababu ya mambo yote mema

18:3 *Maana yake “Mkaaaji Mgeni Huko.” 18:4 *Maana yake “Mungu Wangu Ni Msaidizi.”

ambayo Yehova aliwatendea Waisraeli kwa kuwaokoa kutoka Misri.* **10** Kisha Yethro akasema: “Yehova na asifiwe, aliyekuokoa kutoka Misri na kutoka kwa Farao, na kuwaokoa Waisraeli kutoka mikononi mwa Wamisri. **11** Sasa ninajua kwamba Yehova ni mkuu kuliko miungu mingine yote,^a kwa sababu ya mambo aliyowafanyia wale waliowatendea watu wake kwa kiburi.” **12** Kisha Yethro, baba mkwe wa Musa, akaleta dhahibi ya kuteketezwa na matoleo kwa ajili ya Mungu, na Haruni na wazee wote wa Israeli wakaja kula chakula pamoja na baba mkwe wa Musa, mbele za Mungu wa kweli.

13 Siku iliyofuata, Musa akaketi kama kawaida ili kusikiliza kesi za watu, na watu wakaendelea kuja na kusimama mbele ya Musa tangu asubuhi mpaka jioni. **14** Baba mkwe wake alipoona mambo yote ambayo Musa alikuwa akiwafanyia watu, akamuuliza: “Ni nini hiki unachowafanyia watu? Kwa nini unaketi hapa peke yako huku watu wote wakisimama mbele yako tangu asubuhi mpaka jioni?” **15** Musa akamwambia baba mkwe wake: “Ni kwa sababu watu wanaendelea kuja kwangu kutafuta mwongozo kutoka kwa Mungu. **16** Wakawa na kesi, wanaileta kwangu, nami lazima niamue kesi yao, na kuwajulisha maamuzi ya Mungu wa kweli na sheria zake.”^b

17 Baba mkwe wa Musa akamwambia: “Jambo unalofanya si zuri. **18** Kwa hakika

18:9 *Tnn., “kutoka mkononi mwa Misri.”

SURA YA 18

a Kut 15:11
Zb 95:3
Zb 97:9

b Kum 4:5
Kum 5:1

Safu ya 2

a Yos 1:5,17

b Kut 20:19

c Hes 27:1-5

d Kum 7:11

e Hes 11:16,17
Kum 1:13
Mdo 6:3

f Kut 23:8
ITI 3:2, 3
Tit 1:7
1Pe 5:2

g Kum 1:15
Mdo 14:23

h Law 24:10,11
Hes 15:32,33
Kum 1:17

i Hes 11:17

utachoka, wewe na watu hawa walio pamoja nawe, kwa sababu mzigo huu ni mkubwa sana kwako na huwezi kuubeba peke yako. **19** Sasa nisikilize. Nitakupa ushauri, na Mungu atakuwa pamoja nawe.^a Wewe uwe mwakilishi wa watu mbele za Mungu wa kweli,^b nawe lazima uwasilishe kesi zao mbele za Mungu wa kweli.^c **20** Unapaswa kuwaonya kwa kuwafundisha masharti na sheria,^d na uwajulishe njia wanayopaswa kufuata na kazi wanayopaswa kufanya. **21** Lakini unapaswa kuchagua miongoni mwa watu, wanaume wanaostahili,^e wanaomwogopa Mungu, wanaume wanaotegemea, wanaochukia faida isiyo ya haki,^f nawe uwaweke kuwa wakuu wa maelfu, wakuu wa mamia, wakuu wa hamsini, na wakuu wa makumi.^g **22** Watakuwa waamuzi wa watu kuanapokuwa na kesi,^h nao watakuletea kila kesi iliyo ngumu,^h lakini wao wataamua kila kesi ambayo ni ndogo. Jirahisishie mzigo huu kwa kuwaruhusu wakusaidie kuubeba.ⁱ **23** Ukifanya hivyo, na iwe ndivyo Mungu anavyokuamuru, utaweza kustahimili mkazo huu, na kila mtu atarudi nyumbani akiwa ameridhika.”

24 Mara moja Musa akamsikiliza baba mkwe wake na kufanya yote aliyosema. **25** Musa akachagua wanaume wanaostahili miongoni mwa Waisraeli wote na kuwaweka kuwa viongozi wa watu, kuwa wakuu wa maelfu, wakuu wa mamia, wakuu wa hamsini, na wakuu wa makumi.

18:22 *Tnn., “kila wakati.”

26 Kwa hiyo waliamua kesi walizoletewa na watu. Kesi ngumu walimletea Musa,^a lakini waliamua kila kesi ndogo.

27 Kisha Musa akamuaga baba mkwe wake,^b naye baba mkwe wake akashika njia na kurudi katika nchi yake.

19 Katika mwezi wa tatu baada ya Waisraeli kutoka nchini Misri, siku ileile, walifika katika nyika ya Sinai. **2** Waliondoka Refidimu^c wakafika katika nyika ya Sinai na kupiga kambi nyikani. Waisraeli walipiga kambi huko mbele ya mlima.^d

3 Kisha Musa akapanda mlimani kwa Mungu wa kweli, naye Yehova akamwita kutoka mlimani,^e akamwambia: “Hivi ndivyo utakavyoambia nyumba ya Yakobo na kuwaambia Waisraeli, **4** ‘Mmejionea wenyewe mambo niliyowatendea Wamisri,^f ili niwabebe juu ya mabawa ya tai na kuwaleta kwangu.^g **5** Sasa ikiwa mtaitii kabisa sauti yangu na kushika agano langu, hakika mtakuwa mali yangu ya pekee* kati ya mataifa yote,^h kwa maana dunia yote ni mali yangu.ⁱ **6** Mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani na taifa utakatifu.^j Hayo ndiyo maneno utakayowaambia Waisraeli.”

7 Basi Musa akaenda na kuwaita wazee wote wa Waisraeli na kuwaambia maneno hayo yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru.^k **8** Kisha watu wote wakasema pamoja: “Mambo yote ambayo Yehova amesema, tuko tayari kufanya.”^l Mara moja Musa

19:5 *Au “mali yangu ninayothamini sana.”

SURA YA 18

a Mdo 15:2

b Hes 10:29

SURA YA 19

c Kut 17:1

d Kut 3:1,12

e Mdo 7:38

f Kum 4:34

g Kum 32:11,12
Isa 63:9

h 1Fa 8:53
Zb 135:4

i Kum 10:14

j Law 11:44
Kum 7:6
1Pe 2:9
Ufu 5:9,10

k Kut 24:3

l Kut 24:7
Yos 24:24

Safu ya 2

a Ebr 12:20

b Kut 20:18

c Kut 19:10

d Kum 4:11
1Fa 8:12
Zb 97:2

e Ebr 12:18-21

akamwambia Yehova maneno hayo ambayo watu walisema. **9** Na Yehova akamwambia Musa: “Tazama! nitakujia katika wingu lenye giza, ili watu wasikie ninapozungumza nawe na ili wakuamini wewe pia sikuzote.” Kisha Musa akamwambia Yehova maneno ambayo watu walisema.

10 Halafu Yehova akamwambia Musa: “Nenda uwataka-se watu leo na kesho, nao lazima wafue nguo zao. **11** Nao lazima wawe tayari kwa ajili ya siku ya tatu, kwa sababu katika siku ya tatu mimi Yehova nitashuka juu ya Mlima Sinai mbele ya watu wote. **12** Ni lazima uwawee watu mipaka kuzunguka mlima huu na uwaambie, ‘Jihadharini msipande mlimani wala kugusa ukingo wake. Yeyote atakayeugusa mlima huu hakika atauawa. **13** Mkono wa yeyote usimguse, atapigwa mawe au kuchomwa kwa silaha.* Awe ni mnyama au mwanadamu, hataishi.’^a Lakini pembe ya kondoo dume^b ikipigwa watu wanaweza kuukaribia mlima.”

14 Kisha Musa akashuka kutoka mlimani, akaenda kwa watu, akaanza kuwataka-sa, nao wakafua nguo zao.^c **15** Akawaambia: “Jitayari-sheni kwa ajili ya siku ya tatu. Msifanye ngono.”*

16 Asubuhi, siku ya tatu, kulikuwa na ngurumo na radi, na kulikuwa na wingu zito^d mlimani na sauti kubwa sana ya pembe, na watu wote kambini wakaanza kutetemeka.^e

19:13 *Labda angechomwa kwa mkuki.

19:15 *Tnn., “Msimkaribie mwanamke.”

17 Sasa Musa akawatoa watu nje ya kambi ili wakutane na Mungu wa kweli, nao wakasimama mahali pao chini ya mlima. **18** Mlima Sinai ulifuka moshi kila mahali, kwa sababu Yehova alishuka juu yake katika moto;^a na moshi huo ulikuwa ukipaa kama moshi wa tanuru,* na mlima wote ulikuwa ukitetemeka kwa nguvu sana.^b **19** Sauti ya pembe ilipozidi kuongezeka zaidi na zaidi, Musa akaongea, na sauti ya Mungu wa kweli ikamjibu.

20 Kwa hiyo Yehova akashuka juu ya kilele cha Mlima Sinai. Kisha Yehova akamwita Musa apande juu mlimani, naye Musa akapanda mlimani.^c **21** Sasa Yehova akamwambia Musa: "Shuka chini ukawaonye watu wasijaribu kuvuka mpaka kuja kunitazama mimi, Yehova, la si-vyo wengi wao wataangamia. **22** Nao makuhani wanaonikaribia mimi Yehova kwa ukawaida, wanapaswa kujitakasa, ili mimi, Yehova, nisiwaangamize."^d **23** Basi Musa akamwambia Yehova: "Watu hawawezi kuukaribia Mlima Sinai kwa sababu tayari ulitunya, uliponiambia, 'Weka mipaka kuzunguka mlima huu, ili uwe mtakatifu.'"^e **24** Hata hivyo, Yehova akamwambia: "Nenda, shuka chini, na urudi juu, wewe pamoja na Haruni, lakini usiwaruhusu makuhani na watu wavuke mpaka na kunikaribia mimi Yehova, ili nisiwaangamize."^f **25** Basi Musa akashuka na kuwambia watu maneno hayo.

19:18 *Au "kalibu."

SURA YA 19

a Kut 24:17
Kum 4:11, 12
2Nya 7:1-3

b Zb 68:8

c Kut 24:12

d Law 10:1, 2
1Nya 13:10

e Kut 19:12

f Hes 16:19, 35

Safu ya 2

SURA YA 20

a Kum 5:22
Mdo 7:38

b Kum 5:6
Ho 13:4

c Kum 5:7-10

d Law 26:1
Kum 4:15, 16
Isa 40:25
Mdo 17:29

e Kut 23:24
1Ko 10:20
1Yo 5:21

f Kut 34:14
Mt 4:10
Lu 10:27

g Mhu 12:13

h Law 19:12

i Law 24:15, 16
Kum 5:11

j Kut 16:23
Kut 31:13, 14
Kum 5:12-14

k Kut 23:12

l Kut 16:29
Kut 34:21

20 Kisha Mungu akasema maneno haya yote:^a

2 "Mimi ni Yehova Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa.^b **3** Usiwe na miungu mingine yoyote ila mimi."^c

4 "Usijitengenezee sanamu ya kuchongwa au mfano wa* kitu chochote kilicho juu mbinguni au kilicho chini duniani au kilicho ndani ya maji chini ya dunia.^d **5** Usiviinamie wala kushawishiwa kuviabudu,^e kwa sababu mimi, Yehova Mungu wako, ni Mungu ninayetaka watu waniabudu mimi peke yangu,^f nami huwaadhibu watoto kwa sababu ya makosa ya baba zao, kufikia kizazi cha tatu na kizazi cha nne cha wale wanaonichukia, **6** lakini ninawatendea kwa upendo mshikamanifu watu wanaonipenda na kushika amri zangu, kufikia kizazi cha elfu cha watu hao.^g

7 "Usilitumie jina langu mimi, Yehova Mungu wako, kwa njia isiyofaa,^h kwa maana mimi, Yehova, sitakosa kumwadhibu yule anayetumia jina langu kwa njia isiyofaa.ⁱ

8 "Ikumbuke siku ya Sabato na uione kuwa takatifu.^j **9** Fanya shughuli na kazi zake zote kwa siku sita,^k **10** lakini siku ya saba ni sabato kwa Yehova Mungu wako. Usifanye kazi yoyote, wewe wala mwana wako wala binti yako wala mtumwa wako wala kijakazi wako wala mnyama wako wa kufugwa wala mgeni aliye katika makazi* yako.^l

20:3 *Au "na kuniasi mimi." Tnn., "dhi-di ya uso wangu." 20:4 *Au "umbo la." 20:10 *Tnn., "malango."

11 Kwa maana kwa siku sita mimi, Yehova, niliumba mbinguni na dunia, bahari, na vitu vyote vilivyomo, nami nikaanza kupumzika siku ya saba.^a Ndiyo sababu mimi Yehova niliibariki siku ya Sabato na kufanya kuwa takatifu.

12 “Mheshimu baba yako na mama yako^b ili uishi muda mrefu katika nchi ambayo mimi Yehova Mungu wako ninakupa.^c

13 “Usiue.^d

14 “Usifanye uzinzi.^e

15 “Usiibe.^f

16 “Usitoe ushahidi wa uwongo dhidi wa jirani yako.^g

17 “Usiitamani nyumba ya jirani yako. Usitamani mke wa jirani yako^h wala mtumwa wake wala kijakazi wake wala ng’ombe dume wake wala punda wake wala kitu chochote cha jirani yako.”ⁱ

18 Sasa watu wote walikuwa wakishuhudia ngurumo na radi, sauti ya pembe, na mlima ukifuka moshi; na wali-poona mambo hayo walite-temeka na kusimama mbali.^j

19 Basi wakamwambia Musa: “Wewe ongea nasi, tutasikiliza, lakini Mungu asiongee nasi tusije tukafa.”^k 20 Kwa hiyo Musa akawaambia watu: “Msiogope, kwa sababu Mungu wa kweli amekuja kuwarjaribu,^l ili mwendelee kumwogopa, msitende dhambi.”^m 21 Kwa hiyo watu wakaendelea kusimama mbali, lakini Musa akalikaribia lile wingu jeusi mahali alipokuwa Mungu wa kweli.ⁿ

22 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Hivi ndivyo utakavyoambwa Waisraeli, ‘Mmejionea wenyewe kwamba nimezungumza nanyi kutoka

SURA YA 20

a Mwa 2:2

b Kut 21:15
Law 19:3
Met 1:8

c Kum 5:16
Mt 15:4
Efe 6:2, 3

d Mwa 9:6
Kum 5:17
Yak 2:11
1Yo 3:15
Ufu 21:8

e Mwa 39:7-9
Kum 5:18
Met 6:32
Mt 5:27, 28
Ro 13:9
1Ko 6:18
Ebr 13:4

f Law 19:11
Kum 5:19
Mk 10:19
1Ko 6:9, 10
Efe 4:28

g Law 19:16
Kum 5:20
Kum 19:16-19

h Mt 5:28

i Kum 5:21
Ro 7:7

j Kut 19:16
Ebr 12:18, 19

k Mdo 7:38
Gal 3:19

l Kum 8:2

m Yos 24:14
Ayu 28:28
Met 1:7

n Kum 5:5
Zb 97:2

Safu ya 2

a Kum 4:36
Ne 9:13

b Mdo 17:29

c Kum 12:5, 6
2Nya 6:6

d Kum 27:5
Yos 8:30, 31

SURA YA 21

e Kut 24:3
Kum 4:14

f Law 25:39, 40

g Kum 15:12

h Kum 15:12

i Kum 15:16, 17

mbinguni.^a 23 Msijitengenezee miungu ya fedha na kuia-budu huku mkiniabudu mimi, wala msijitengenezee miungu ya dhahabu.^b 24 Mtanijengea madhabahu ya udongo, na juu yake mtanitolea dhahabu zenu za kuteketezwa, dhahabu zenu za ushirika,^c kondo, mbuzi, na ng’ombe wenu. Mahali popote nitakapochagua jina langu likumbukwe,^c nitawajia, nami nitawabariki. 25 Ikiwa mtanijengea madhabahu ya mawe, msijenge kwa mawe yaliyokatwa kwa vifaa.^{*d} Kwa maana mkiyachonga kwa tindo, mtaitia madhabahu hiyo unajisi. 26 Nanyi msipande madhabahu yangu kwa ngazi, ili sehemu zenu za siri zisionekane* juu yake.’

21 “Hizi ndizo sheria utakazowapa* Waisraeli:^e

2 “Ukimnunua mtumwa Mwebrania,^f atakuwa mtumwa kwa miaka sita, lakini mwaka wa saba, utamweka huru, naye hatalipa chochote.^g

3 Ikiwa alikuja peke yake, ataondoka peke yake. Ikiwa ana mke, basi mke wake anapaswa kuondoka naye. 4 Ikiwa bwana wake atampa mke, na mke huyo amzalie wana au mabinti, mke huyo na watoto wake watakuwa mali ya bwana wake, na mtumwa huyo ataondoka peke yake.^h 5 Lakini mtumwa huyo akisisitiza hivi: ‘Nampenda bwana wangu, mke wangu, na wanangu; sitaki kuachiliwa huru,’ⁱ 6 ni lazima bwana wake amle-

20:24 *Au “matoleo yenu ya amani.”

20:25 *Au “yaliyochongwa.” 20:26 *Tnn., “uchi wenu usionekane.” 21:1

*Tnn., “Haya ndiyo maamuzi ya hukumu utakayowapa.”

te mbele za Mungu wa kweli. Kisha bwana huyo atamleta kwenye mlango au kwenye mwimo wa mlango na kulitoboa sikio lake kwa sindano, naye atakuwa mtumwa wake maisha yake yote.

7 “Mtu akimuuza binti yake kuwa mtumwa, hataondoka kama mtumwa wa kiume anavyoondoka. 8 Ikiwa bwana wake hapendezwi naye na hataki awe suria wake, lakini aamue kumuza kwa mtu mwingine,* bwana huyo hana haki ya kumuza kwa wageni kwa sababu amemsaliti mtumwa huyo. 9 Akimchagua awe mke wa mwanawe, anapawisa kumpa haki anazostahili kama binti yake. 10 Ikiwa ataoa mke mwingine, hapaswi kumpunguzia mke huyo wa kwanza chakula, mavazi, na haki yake ya ndoa.^a 11 Ikiwa hatampa mambo hayo matau, basi mtumwa huyo wa kike ataondoka bila kulipa pesa zozote.

12 “Yeyote anayempiga mtu na kumuua lazima auawe.^b 13 Lakini ikiwa alimua bila kukusudia na Mungu wa kweli akaruhusu jambo hilo litokee, basi nitawaonyesha mahali anapoweza kukimbilia.^c 14 Mtu akimkasirikia vikali mwenzake na kumuua kwa kukusudia,^d mtu huyo lazima afe hata ikiwalazimu kumwondoa kwenye madhabahu yangu.^e 15 Mtu anayempiga baba yake au mama yake lazima auawe.^f

16 “Yeyote anayemteka nyara mtu mwingine^g na kumuza au akipatikana amemzuilia,^h lazima auawe.ⁱ

21:8 *Tnn., “akombolewe.”

SURA YA 21

a 1Ko 7:3

b Mwa 9:6
Hes 35:30
Mt 5:21

c Hes 35:11
Hes 35:22-25
Kum 4:42
Kum 19:3-5
Yos 20:7-9

d Hes 15:30

e Kum 19:11, 12
1Fa 1:50
1Fa 2:29
1Yo 3:15

f Kut 20:12

g Mwa 40:15

h Mwa 37:28

i Kum 24:7

Safu ya 2

a Law 20:9
Met 20:20
Met 30:11, 17
Mt 15:4

b Mwa 9:5, 6
Law 24:17

c Zb 139:16
Yer 1:5

d Kut 18:25, 26
Kum 16:18
Kum 17:8

e Mwa 9:6
Law 24:17
Hes 35:31
Ufu 21:8

f Law 24:20
Mt 5:38

17 “Yeyote anayemlaani baba yake au mama yake lazima auawe.^a

18 “Hivi ndivyo mtakavyofanya wanaume wakigombana na mmoja wao ampige mwenzake kwa jiwe au ngumi* lakini asimuuze bali amjeruhi hivi kwamba ashindwe kutoka kitandani: 19 Ikiwa anaweza kutoka kitandani na kuteembea nje kwa kutumia fimbo, basi yule aliyempiga hataadhibiwa. Atamlipa tu fidia kwa ajili ya wakati aliopoteza alipokuwa kitandani mpaaka atakapopona kabisa.

20 “Mtu akimpiga kwa fimbo mtumwa wake wa kiume au wa kike naye afie mikononi mwake, ni lazima mtumwa huyo alipiziwe kisasi.^b 21 Hata hivyo, mtumwa huyo akiendelea kuishi kwa siku moja au siku mbili, hatalipiziwa kisasi, kwa sababu alinunuliwa kwa pesa za bwana wake.

22 “Wanaume wakipambana na kumuumiza mwanamke mwenye mimba naye azae kabla ya wakati*^c lakini kifo kisitokee,^d yule aliyemuumiza atalipa hasara atakayodaiwa na mume wa mwanamke huyo; naye atalipa kupitia waumuzi.^d 23 Lakini kifo kikitokea, basi ni lazima mlipye uhai kwa uhai,^e 24 jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu,^f 25 alama ya moto kwa alama ya moto, jeraha kwa jeraha, pigo kwa pigo.

26 “Mtu akilipiga jicho la mtumwa wake wa kiume au

21:18 *Au labda, “kwa kifaa.” 21:22 *Tnn., “na watoto wake watoke tumboni.” #Au “na kusiwepo na majeraha mabaya.” 21:23 *Au “nafsi kwa nafsi.”

jicho la mtumwa wake wa kike na kuliharibu, atamwachilia huru mtumwa huyo ili kufidia jicho lake.^a **27** Naye akimpiga na kumng'oa jino mtumwa wake wa kiume au wa kike, atamwachilia huru mtumwa huyo ili kufidia jino lake.

28 "Ng'ombe dume akimpiga pembe mwanamume au mwanamke na kumuua, ng'ombe dume huyo atauawa kwa kupigwa mawe^b na nyama yake haipaswi kulwa; lakini mwenye ng'ombe dume huyo hataadhibiwa. **29** Lakini ikiwa ng'ombe dume alizoea kuwapiga watu pembe na mwenyewe akaonywa lakini hakumfunga, naye amuue mwanamume au mwanamke, ng'ombe dume huyo anapaswa kupigwa mawe na mwenye ng'ombe dume huyo anapaswa kuuawa pia. **30** Ikiwa atadaiwa fidia,* atalipa chochote atakachodaiwa ili kuko-mboa uhai wake.[#] **31** Ng'ombe dume huyo akimpiga pembe mtoto wa kiume au wa kike, mwenye ng'ombe dume huyo atattendewa kulingana na sheria hii. **32** Ng'ombe dume huyo akimpiga pembe mtumwa wa kiume au wa kike, mwenye ng'ombe dume huyo atamlipa bwana wa mtumwa huyo shekeli 30,* na ng'ombe dume huyo atauawa kwa kupigwa mawe.

33 "Mtu akiacha shimo wazi au akichimba shimo na kukosa kulifunika, na ng'ombe dume au punda aanguke humo, **34** mwenye shimo hilo atalipa fidia.^c Atamli-

21:30 *Au "ridhaa." #Au "nafsi yake."
21:32 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 21

a Efe 6:9
Kol 4:1

b Mwa 9:5
Hes 35:33

c Kut 22:6
Kut 22:14
Kum 22:8

Safu ya 2

SURA YA 22

a 2Sa 12:6
Lu 19:8

b Kut 20:15

pa mwenye mnyama huyo, na mnyama aliyekufa atakuwa wake. **35** Ng'ombe dume aki-muumiza na kumuua ng'ombe dume wa mtu mwingine, basi watamuza ng'ombe dume aliyehai na kugawana pesa hizo; wanapaswa pia kugawana ng'ombe aliyekufa. **36** Au ikiwa ilijulikana kwamba ng'ombe dume alizoea kupiga kwa pembe lakini mwenye ng'ombe dume huyo hakumfunga, lazima alipe ng'ombe dume kwa ng'ombe dume, kisha ng'ombe dume aliyekufa atakuwa wake.

22 "Mtu akiiba ng'ombe dume au kondoo na kumchinja au kumuua, atalipa ng'ombe dume watano kwa ajili ya ng'ombe dume huyo na kondoo wanne kwa ajili ya kondoo huyo.^a

2 ("Mwizi^b akipatikana aki-vunja nyumba kisha apigwe na kufa, aliyemuua hatakuwa na hatia ya damu. **3** Lakini jambo hilo likitokea baada ya jua kuchomoza, atakuwa na hatia ya damu.)

"Anapaswa kulipa. Ikiwa hana chochote, basi atauzwa ili kulipia vitu alivyoiba. **4** Kama mnyama aliyeibwa anapatikana akiwa hai mikononi mwake, awe ni ng'ombe dume au punda au kondoo, anapaswa kulipa mara mbili.

5 "Mtu yeyote akiwalisha wanyama wake katika shamba au shamba la mizabibu la mtu mwingine, atalipa kwa mazao bora ya shamba lake mwenyewe au mazao bora ya shamba lake mwenyewe la mizabibu.

6 "Moto ukiwaka na kuenea katika vichaka vya miiba na kuteketeza masuke au nafa-ka iliyo shambani au shamba,

yule aliyewasha moto huo lazima alipie kilichoteketea.

7 “Mtu akimpa jirani yake pesa au vitu amtunzie, navyo viibwe kutoka katika nyumba ya jirani huyo, mwizi akipatikana, lazima alipe mara mbili.^a **8** Mwizi asipatikana, mwenye nyumba atale-twa mbele za Mungu wa kweli^b ili ithibitishwe ikiwa alichukua vitu vya jirani yake au la. **9** Katika visa vyote vya kumiliki vitu isivyo halali, iwe ni ng’ombe dume, punda, kondoo, nguo, au kitu chochote kilichopotea ambacho hueda mtu akasema, ‘Hiki ni changu!’ wote wawili wataleta kesi yao mbele za Mungu wa kweli.^c Yule ambaye Mungu atasema ana hatia atamlipa jirani yake mara mbili.^d

10 “Mtu akimpa jirani yake punda au ng’ombe dume au kondoo au mnyama yeyote wa kufugwa amtunzie, kisha mnyama huyo afe au alemazwe au achukuliwe bila mtu yeyote kuona, **11** yule aliye-pewa mali hiyo ataapa mbele za Yehova kwamba haku-chukua mali ya jirani yake; na mwenye mali anapaswa kukubali jambo hilo. Mtu huyo hatalipa chochote.^e **12** Lakini ikiwa mnyama huyo ameibwa kutoka kwake, atamlipa mwenye mnyama huyo. **13** Ikiwa mnyama huyo aliraruliwa na mnyama wa mwituni, atamleta kama ushahidi. Hatalipia kitu kilichoraruliwa na mnyama wa mwituni.

14 “Lakini mtu yeyote akiazima mnyama kutoka kwa jirani yake, na mnyama huyo alemazwe au afe wakati mwenyewe hayupo, aliyeezima mnyama huyo lazima alipe.

SURA YA 22

a Kut 22:4

b Kum 16:18
Kum 19:17

c Kum 16:18
Kum 25:1

d Kut 22:4

e Law 6:2-5

Safu ya 2

a Kum 22:28, 29

b Law 19:26
Law 20:6
Kum 18:10-12
1Sa 28:3
Gal 5:20
Ufu 22:15

c Law 18:23
Law 20:15
Kum 27:21

d Hes 25:3
1Fa 18:40
1Ko 10:20

e Law 25:35

f Law 19:33, 34
Kum 10:19

g Kum 27:19
Yak 1:27

h Zb 10:18
Yak 5:4

i Law 25:35, 36
Kum 23:19
Lu 6:34, 35

j Kum 24:6

15 Ikiwa mwenyewe yupo, aliyeezima hatalipa. Ikiwa mnyama huyo alikodiwa, pesa iliyo-lipwa ili kumkodi ndiyo itakayokuwa malipo yake.

16 “Sasa mwanamume aki-mtongoza bikira ambaye hachumbiwa kisha alale naye, lazima alipe mahari ili msichana huyo awe mke wake.^a

17 Baba yake akikataa kabisa kumpa msichana huyo, mwanamume huyo atalipa kiasi cha pesa kinacholingana na mahari.

18 “Hampaswi kumwacha mwanamke mchawi aishi.^b

19 “Mtu yeyote anayefanya ngono na mnyama lazima auawe.^c

20 “Mtu yeyote anayetoa dhabihu kwa miungu mingine isipokuwa kwa Yehova peke yake lazima auawe.^d

21 “Msimtese wala kumkandamiza mkaaji mgeni,^e kwa sababu ninyi mlikuwa wakaa-ji wageni katika nchi ya Misri.^f

22 “Msimtese mjane wala yatima.^g **23** Mkimtesa hata kidogo, naye anililie, hakika nitasikia kilio chake;^h

24 nami nitawaka hasira, nami nitawaua kwa upanga, na wake zenu watakuwa wajane, na watoto wenu watakuwa mayatima.

25 “Ukimkopesha pesa mtu yeyote maskini miongoni mwa watu wangu, mtu anayeishi nawe, usiwe kama mtu anayemkopesha pesa.* Hupaswi kumtoza riba.ⁱ

26 “Ukichukua nguo ya jirani yako kuwa dhamana ya mkopo,^{*j} unapaswa kumrudishia kabla ya jua kutua.

22:25 *Au “mla riba.” 22:26 *Au “rehani.”

27 Kwa sababu hiyo ndiyo nguo pekee aliyo nayo ya kuji-funika, nguo ya kufunika mwili wake,* atajifunikia nini anapolala?^a Akinililia, hakika nitasikia, kwa sababu mimi ni mwenye huruma.^{#b}

28 "Usimtukane Mungu^c wala kumlaani kiongozi* miongoni mwa watu wako.^d

29 "Usisite kutoa matoleo kutoka katika mazao yako mengi na kutoka kwenye mafuriko ya mashinikizo yako.*^e Unapaswa kunipa mzaliwa wa kwanza kati ya wanao.^f

30 Hivi ndivyo utakavyofanya kuhusu ng'ombe dume wako na kondoo wako:^g Atakaa na mama yake kwa siku saba. Siku ya nane, utanipa mimi.^h

31 "Mnapaswa kujithibiti-sha wenyewe kuwa watu watakatifu mbele zangu,ⁱ nanyi hamipaswi kula nyama ya mnyama yeyote ambaye ameraruliwa na mnyama wa mwituni.^j Mnapaswa kuwatupia mbwa nyama hiyo.

23 "Usieneze habari za uwongo.^k Usishirikiane na mtu mwovu kwa kutoa ushahidi utakaowadhuru wengine.^l 2 Usiufuate umati ili kutenda maovu, wala usipot-she haki kwa kutoa ushahidi wa uwongo ili uunge mkono umati.* 3 Usionyeshe upe-ndeleo katika kesi ya mtu maskini.^m

4 "Ukikutana na ng'ombe dume au punda wa adui yako akitangatanga, unapaswa kumrudisha kwake.ⁿ 5 Uki-

22:27 *Tnn., "ngozi yake." #Au "nee-ma." 22:28 *Au "mtawala." 22:29 *Yaani, mashinikizo ya mafuta na mashinikizo ya divai. 23:2 *Au "ushahidi unaoungwa mkono na wengi."

SURA YA 22

a Kum 24:13

b Kum 10:18
Zb 34:6

c Law 24:11, 14

d Mhu 10:20
Mdo 23:5
Yud 8e Met 3:9
2Ko 9:7

f Kut 13:2

g Kum 15:19

h Law 22:27

i Law 19:2
Hes 15:40
1Pe 1:15

j Law 22:3, 8

SURA YA 23

k Law 19:16
Met 6:16, 19l Kum 19:18, 19
Met 19:5

m Law 19:15

n Met 25:21
1Th 5:15

Safu ya 2

a Kum 22:4
Lu 6:27
Ro 12:21b Kum 16:19
2Nya 19:7c Met 17:15
Ro 1:18
Ro 2:6

d Mhu 7:7

e Law 19:34

f Law 25:3, 4

g Kut 20:9, 10
Kum 5:14

mwona punda wa mtu anayekuchukia amelemewa na mzi-go na kuanguka, usimpuuzi na kusenda zako. Unapaswa kumsaidia kufungua mnyama huyo.^a

6 "Usipotoshe uamuzi wa kesi ya maskini aliye miongoni mwenu.^b

7 "Jiepushe kabisa na shtaka* la uwongo, na usimuue mtu asiye na hatia na pia mwadilifu, kwa maana sita-mtangaza mwovu kuwa mwadilifu.^{#c}

8 "Hupaswi kukubali rushwa, kwa maana rushwa huwapofusha watu wanao-na vizuri na inaweza kupotosha maneno ya watu wenye haki.^d

9 "Hupaswi kumkandamiza mkaaaji mgeni. Mnajua jinsi mgeni anavyohisi,* kwa sababu mlikuwa wakaaji wageni katika nchi ya Misri.^e

10 "Kwa miaka sita utapanda mbegu katika shamba lako na kuvuna mazao yake.^f

11 Lakini mwaka wa saba hutalilima, utaliacha lipumzike, nao maskini walio miongoni mwa watu wako watapata chakula humo, na watakachoa-cha kitaliwa na wanyama wa mwituni. Hivyo ndivyo utakavyolifanyia shamba lako la mizabibu na shamba lako la mizeituni.

12 "Kwa siku sita utafanya kazi zako; lakini siku ya saba hutafanya kazi, ili ng'ombe dume wako na punda wako wapumzike na mwana wa kijakazi wako na mkaaaji mgeni waweze kujiburudisha.^g

23:7 *Tnn., "neno." #Au "sitamwondolea mashtaka mtu mwovu." 23:9 *Au "Mnajua maisha (nafsi) ya mgeni."

13 “Unapaswa kuwa mwanalifu kufanya mambo yote niliyokuambia,^a nawe hupaswi kutaja majina ya miungu mingine; yasisikike midomoni^{*b} mwako.

14 “Unapaswa kunifanyia sherehe mara tatu kwa mwaka.^c **15** Utaadhimisha Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu.^d Utakula mikate isiyo na chachu kwa siku saba, kama nilivyokuamuru, wakati uliowekwa katika mwezi wa Abibu,^{*e} kwa sababu ulitoka Misri wakati huo. Mtu yeyote asije mbele zangu mikono mitupu.^f

16 Pia, unapaswa kuadhimisha Sherehe ya Mavuno^{*g} ya matunda ya kwanza yaliyoiva[#] ya kazi zako, na ya vitu unavyopanda shambani;^g na Sherehe ya Kukusanya^Δ mwishoni mwa mwaka, unapokusanya mazao ya kazi zako.^h **17** Mara tatu kwa mwaka wanaume wako wote wanapaswa kuja mbele za Bwana wa kweli, Yehova.ⁱ

18 “Hupaswi kutoa damu ya dhahihu yangu pamoja na kitu chochote kilichotiwa chachu. Na dhahihu za mafuta zinazotolewa katika sherehe zangu hazipaswi kukaa usiku kucha mpaka asubuhi.

19 “Unapaswa kuleta katika nyumba yangu mimi, Yehova Mungu wako, mazao bora ya kwanza yaliyokomaa^{*} ya ardhi yako.^j

“Usimchamshe mwanambuzi katika maziwa ya mama yake.^k

23:13 *Tnn., “kinywani.” **23:15** *Angalia Nyongeza B15. **23:16** *Pia inaitwa Sherehe ya Majuma, au Pentekoste. [#]Au “mazao ya kwanza yaliyokomaa.” ^ΔPia inaitwa Sherehe ya Vibanda (Mahe-ma). **23:19** *Au “matunda ya kwanza bora yaliyoiva.”

SURA YA 23

a Kum 4:9

b Kum 12:3
Yos 23:6, 7

c Kum 16:16

d Law 23:6
Lu 22:7

e Kut 12:18

f Kum 16:17

g Hes 28:26
Kum 16:9, 10
Mdo 2:1h Kum 16:13
Ne 8:14
Yoh 7:2

i Kum 12:5, 6

j Hes 18:8, 12
1Ko 15:20k Kum 14:21
Met 12:10

Safu ya 2

a Kut 14:19

b Hes 20:16

c Hes 14:35
Yos 24:19d Kut 34:11
Yos 5:13, 14
Yos 24:8e Kut 20:5
Law 18:3
Kum 12:30
2Nya 33:2f Kut 20:3
Hes 33:52g Kum 6:13
Kum 10:12
Yos 22:5
Mt 4:10

h Kum 7:13

i Kum 7:15

j Kum 7:14
Kum 28:4k Kum 2:25
Yos 2:9

l Kum 7:23, 24

m Kum 7:20
Yos 2:11

20 “Ninamtuma malaika awatangulie^a ili awalinde safarini na kuwapeleka mahali nilipotayarisha.^b **21** Msikilizeni, na mtii sauti yake. Msimwasi, kwa maana hatawasamehe maasi yenu,^c kwa sababu jina langu limo ndani yake. **22** Hata hivyo, mkiitii kabisa sauti yake na kufanya yote ninayowaambia, nitakuwa adui wa maadui wenu na kuwapinga wale wanaowapinga. **23** Kwa maana malaika wangu atawatangulia na kuwapeleka katika nchi ya Waamori, Wahiti, Waperizi, Wakanaani, Wahivi, na Wayebusi, nami nitawaangamiza.^d **24** Hampaswi kuiinamia miungu yao wala kushawishiwa kuiabudu, nanyi hampaswi kuiga mazoea yao.^e Bada la yake, mnapaswa kuharibu kabisa sanamu zao na kuvunjavunja nguzo zao takatifu.^f **25** Mnapaswa kunitumikia mimi, Yehova Mungu wenu,^g nami nitabariki mka-te wenu na maji yenu.^h Nitao-ndoa magonjwa miongoni mwenu.ⁱ **26** Hakuna mwana-mke katika nchi yenu ambaye mimba yake itaharibika wala atakayekuwa tasa,^j nami nitawapa maisha marefu.^{*}

27 “Nitafanya watu wanio-gope hata kabla hamjafika,^k nami nitawavuruga watu wote mtakaokutana nao, nami nitawafanya maadui wenu wote washindwe na kukimbia.^{*l} **28** Nitawafanya Wahivi, Wakanaani, na Wahiti wavunjike moyo^{*} kabla hamjafika,^m

23:26 *Au “nitafanya idadi ya siku zenu iwe kamili.” **23:27** *Au “nitawafanya maadui wenu wote wawageuzie mgongo.” **23:28** *Au labda, “washikwe na wasiwasi; waogope.”

nao watawakimbia.^a **29** Sitawafukuza watoke mbele yenu kwa mwaka mmoja, ili nchi isibaki ukiwa na wanyama wa mwituni waongezeke na kuwashambulia.^b **30** Nitawafukuza hatua kwa hatua kutoka mbele yenu, mpaka mtaka-poongezeka na kuwa wengi na kuimiliki nchi hiyo.^c

31 "Nitaweka mpaka wenu kuanzia Bahari Nyekundu mpaka bahari ya Wafilisti na kuanzia nyikani mpaka kwenye Mto Efrati,^d kwa maana nitawatia wakaaji wa nchi hiyo mikononi mwenu, nanyi mtawafukuza kutoka mbele yenu.^e **32** Hampaswi kufanya agano pamoja nao wala na miungu yao.^f **33** Hawapaswi kuishi katika nchi yenu, wasije wakasababisha mnitende dhambi. Mkiiabudu miungu yao, kwa hakika itakuwa mtego kwenu."^g

24 Kisha akamwambia Musa: "Panda uje kwangu mimi Yehova, wewe na Haruni, Nadabu na Abihu,^h na wazee 70 wa Israeli, nanyi mwiname chini mkiwa mbali. **2** Musa anapaswa kunikaribia mimi, Yehova, akiwa peke yake; lakini wale wengine hawapaswi kunikaribia, na watu hawapaswi kupanda pamoja naye."ⁱ

3 Kisha Musa akaja na kuwambia watu maneno yote ya Yehova na sheria zote,^{*j} na watu wote wakajibu hivi kwa sauti moja: "Maneno yote ambayo Yehova amesema, tuko tayari kuyafanya."^k

4 Basi Musa akaandika maneno yote ya Yehova.^l Kisha akaamka asubuhi na mapema na kujenga madhabahu kwe-

SURA YA 23

a Yos 24:11

b Kum 7:22

c Kum 9:4

d Mwa 15:18
Kum 1:7
Yos 1:4
1Fa 4:21e Amu 1:4
Amu 11:21f Kut 34:12
Hes 25:1, 2
Kum 7:2
2Ko 6:14g Yos 23:12, 13
Amu 1:28
Zb 106:36

SURA YA 24

h Law 10:1

i Kut 20:21
Hes 12:8j Kut 21:1
Kum 4:1k Kum 5:27
Yos 24:22l Kut 34:27
Kum 31:9

Safu ya 2

a Law 3:1
Law 7:11b Kum 31:11
Mdo 13:15

c Kut 19:8

d Ebr 12:24

e Ebr 9:18-20

f Yoh 1:18

g Eze 1:26
Ufu 4:3

h Kut 24:1

i Kum 5:22

j Hes 11:28

nye sehemu ya chini ya mlima huo na nguzo 12 kulingana na idadi ya makabila 12 ya Israeli. **5** Baada ya hayo akawatuma wanaume vijana Waisraeli, nao wakatoa dhahihu za kuteketezwa na dhahihu za ng'ombe dume ili ziwe dhahihu za ushirika^a kwa Yehova. **6** Kisha Musa akachukua nusu ya damu ya wanyama hao na kuitia ndani ya mabakuli, na nusu ya damu hiyo akainyunyiza kwenye madhabahu. **7** Halafu akachukua kitabu cha agano na kuwasomea watu kwa sauti.^b Nao wakasema: "Mambo yote ambayo Yehova amesema tuko tayari kuyafanya, nasi tutatii."^c **8** Basi Musa akachukua damu akawanyunyizia watu^d na kusema: "Hii ndiyo damu ya agano ambalo Yehova amefanya pamoja nanyi kulingana na maneno hayo yote."^e

9 Musa na Haruni, Nadabu na Abihu, na wazee 70 wa Israeli wakapanda mlimani, **10** nao wakamwona Mungu wa Israeli.^f Chini ya miguu yake palikuwa na kitu kilichoonekana kama saku ya yakuti, nacho kilikuwa safi kama mbingu zenyewe.^g **11** Hakuwadhuru wanaume hao wenye kuheshimika wa Israeli,^h nao walipata maono ya Mungu wa kweli, wakala na kunywa.

12 Sasa Yehova akamwambia Musa: "Panda uje kwangu mlimani na ukae huku. Nitakupa mabamba ya mawe yenye sheria na amri nitakazoandika ili kuwafundisha watu."ⁱ **13** Basi Musa akaondoka pamoja na Yohua mhdumu wake,^j naye Musa akapanda kwenye mlima wa

Mungu wa kweli.^a **14** Lakin ali kuwa amewaambia wale wazee: “Tungojeeni hapa mpaka tutakaporudi.^b Haruni na Huru^c wako pamoja nanyi. Yeyote aliye na kesi anaweza kuwapelekea.”^d **15** Ndipo Musa akapanda mlimani wingu lilipokuwa likiufunika mlima huo.^e

16 Utukufu wa Yehova^f ulienelea kukaa juu ya Mlima Sinai,^g na wingu likaufunika kwa siku sita. Siku ya saba akamwita Musa kutoka kati kati ya lile wingu. **17** Kwa Waisraeli waliokuwa wakitamzama, utukufu wa Yehova ulionekana kama moto mkali kwenye kilele cha mlima. **18** Ndipo Musa akaingia ndani ya lile wingu na kupanda mlimani.^h Musa akakaa mlimani siku 40, mchana na usiku.ⁱ

25 Kisha Yehova akamwambia Musa: **2** “Waa mbie Waisraeli wanitolee mchango; mnapaswa kuchukua mchango wangu kutoka kwa kila mtu ambaye moyo wake unamchochea kuchanga.^j **3** Huu ndio mchango utakaopokea kutoka kwao: dhahabu,^k fedha,^l shaba,^m **4** nyuzi za bluu, sufu ya zambarau,ⁿ kitambaa cha rangi nyekundu,^o kitani bora, manyoya ya mbuzi, **5** ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu, ngozi za sili,^p mbao za mshita,^q **6** mafuta kwa ajili ya taa,^r mafuta ya zeri ya kutengenezea mafuta yanayotumiwa kutia mafuta^s na kwa ajili ya uvumba uliotiwa manu-

25:4 *Au “sufu iliyotiwa rangi ya zambarau.” ^aRangi hiyo ilitoka kwa mdu du anayeitwa kochinili. **25:5** *Mnyama wa baharini.

SURA YA 24

a Kut 24:2

b Kut 32:1

c Kut 17:10

d Kut 18:25, 26

e Kut 19:9

f Kut 16:10
Law 9:23
Hes 16:42

g Kut 19:11

h Kut 19:20

i Kut 34:28
Kum 9:9

SURA YA 25

j Kut 35:4-9
1Nya 29:9
2Ko 9:7

k Kut 38:24

l Kut 38:25

m Kut 38:3
Kut 38:29

n Kut 36:20

o Kut 27:20

p Kut 30:23-25

Safu ya 2

a Kut 30:34, 35

b Kut 28:6

c Kut 28:15

d Kut 29:45
1Fa 6:13
Ebr 9:11e 1Nya 28:12
Mdo 7:44
Ebr 8:5
Ebr 9:9

f Kut 37:1-5

g Ebr 9:4

h Kut 30:1, 3

i Kut 30:1, 5
1Nya 15:15

j 1Fa 8:8

k Kut 31:18
Kut 40:20
1Fa 8:9
Ebr 9:4

l Kut 37:6-9

kato,^a **7** na mawe ya shohamu na mawe mengine ya kupambia efodi^b na kifuko cha kifuni.^c **8** Mtanjengea mahali patakatifu, nami nitakaa* miongoni mwenu.^d **9** Mtatengeza mahali hapo patakatifu, yaani, hema la ibada pamoja na vyombo vyake vyote, mki fuata kikamili kielelezo nitakachowaonyesha.*^e

10 “Mtanjengezea sanduku la mbao za mshita lenye urefu wa mikono miwili na nusu* na upana wa mkono mmoja na nusu na kimo cha mkono mmoja na nusu.^f **11** Kisha utalifunika kwa dhahabu safi.^g Utalifunika ndani na nje na kutengeneza ukingo wa dhahabu kulizunguka.^h **12** Nawe utatengeza pete nne za dhahabu na kuzifunga sehemu ya juu ya miguu yake minne, pete mbili upande mmoja na pete mbili upande wa pili. **13** Nawe utatengeneza fito za mshita na kuzifunika kwa dhahabu.ⁱ **14** Utazitia fito hizo katika zile pete zilizo kwenye pande mbili za Sanduku ili zitumiwe kulibeba. **15** Fito hizo zitakaa kwenye pete za Sanduku; hazipaswi kuondolewa.^j **16** Nawe utaweka ndani ya sanduku hilo mabamba ya ushahidi nitakayokupa.^k

17 “Utatengeneza kifuniko cha dhahabu safi chenye urefu wa mikono miwili na nusu na upana wa mkono mmoja na nusu.^l **18** Nawe utatengeneza makerubi wawili wa dhahabu; utawatengeneza kwa

25:8 *Au “nitapiga hema.” **25:9** *Au “mchoro nitakawaonyesha.” **25:10** *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

nyundo kwenye miisho miwili ya kifuniko hicho.^a **19** Tengeneza kerubi mmoja kwenye mwisho mmoja na kerubi mwingine kwenye mwisho wa pili wa kifuniko. **20** Makerubi hao watakuwa wamenyoosha mabawa yao mawili kuelekea juu, na hivyo kukifunika kifuniko hicho kwa mabawa yao,^b nao wataelekeana. Nyuso za makerubi hao zitatazama kifuniko. **21** Utakiweka kifuniko^c hicho juu ya Sanduku, na ndani ya Sanduku utaweka mabamba ya ushahidi nitakayokupa. **22** Nitakutokea hapo na kuzungumza nawe kutoka juu ya kifuniko hicho.^d Kutoka katikati ya hao makerubi wawili walio juu ya sanduku la Ushahidi, nitakujulisha amri zote utakazowapa Waisraeli.

23 "Pia utatengeneza meza^e ya mbao za mshita yenye urefu wa mikono miwili na upana wa mkono mmoja na kimo cha mkono mmoja na nusu.^f **24** Utaifunika kwa dhahabu safi na kutengeneza ukingo wa dhahabu kuizunguka. **25** Utatengeneza utepe wenyewe upana wa kiganja kimoja* kuizunguka na ukingo wa dhahabu kuzunguka utepe huo. **26** Utaitengeneza pete nne za dhahabu na kuzitia kwenye pembe nne za miguu yake minne, sehemu ambazo miguu hiyo minne inaungana na meza. **27** Pete hizo zitakuwa karibu na utepe ili zitiwe fito za kubebea meza hiyo. **28** Utatengeneza fito za mshita na kuzifunika kwa dhahabu, nanyi mtazitumia kubebea meza hiyo.

25:25 *Karibu sentimita 7.4 (inchi 2.9). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 25

a 1Sa 4:4
Ebr 9:5

b 1Fa 8:7
1Nya 28:18

c Kut 40:20
Ebr 9:4, 5

d Kut 30:6
Law 16:2
Hes 7:89
Amu 20:27
Zb 80:1

e Kut 40:22
Law 24:6
Hes 3:30, 31
Ebr 9:2

f Kut 37:10-15

Safu ya 2

a Kut 37:16
Hes 4:7
1Fa 7:48, 50

b Law 24:5, 6
1Sa 21:6
1Nya 9:32
2Nya 13:11
Mt 12:4

c Kut 40:24
1Fa 7:48, 49
Ebr 9:2

d Kut 37:17-24

e Hes 8:4

f Kut 30:8
Law 24:2, 3
Hes 8:2
2Nya 13:11

g Hes 4:9

29 "Pia utatengeneza sahani, vikombe, magudulia, na mabakuli ya meza hiyo, vitu ambavyo watatumia kumimina matoleo ya vinywaji. Utatengeneza vyombo hivyo kwa dhahabu safi.^a **30** Nawe utaweka mikate ya wonyesho juu ya meza hiyo ili iwe mbele zangu daima.^b

31 "Utatengeneza kinara cha taa^c cha dhahabu safi. Kinara hicho cha taa kitatengenezwa kwa nyundo. Sehemu yake ya chini, shina lake, matawi yake, vikombe vyake, matumba yake, na maua yake yatatengenezwa kwa kipande kimoja cha dhahabu.^d **32** Kinara hicho kitakuwa na matawi sita, matawi matatu upande mmoja na matawi matatu upande wa pili. **33** Kila tawi litakuwa na vikombe vitatu vyenye umbo la maua ya mlozi; kila kikombe kitakuwa na ua na tumba lake. Hivyo ndivyo matawi hayo sita yatakavyotengenezwa kwenye shina la kinara hicho cha taa. **34** Kwenye shina la kinara hicho utatengeneza vikombe vinne vyenye umbo la maua ya mlozi, kila kikombe kitakuwa na ua na tumba lake. **35** Kutakuwa na tumba chini ya jozi wa kwanza ya matawi hayo sita, tumba chini ya jozi ya pili, na tumba chini ya jozi ya tatu. **36** Matumba na matawi yake na kinara chote cha taa kitatengenezwa kwa kipande kimoja cha dhahabu safi, kwa kutumia nyundo.^e **37** Utatengeneza taa saba kwa ajili ya kinara hicho, na taa hizo zinapowashwa zitaangaza mbele ya kinara hicho.^f **38** Koleo zake na vyetezo vyake vitatengenezwa kwa dhahabu safi.^g

39 Kinara hicho, pamoja na vifaa hivyo vinapaswa kute-ngenezwa kwa talanta moja* ya dhahabu safi. **40** Hakikisha kwamba unatengeneza vitu hivyo kwa kufuata kielelezo* ulichoonyeshwa mli-mani.^a

26 “Utatengeneza hema la ibada^b kwa vitambaa kumi vya kitani bora kili-chosokotwa, pia kwa nyuzi za bluu, sufu wa zambarau, na kitambaa cha rangi nyekundu. Utavitarizi^c kwa michoro^d ya makerubi. **2** Kila kitambaa cha hema la ibada kita-kuwa na urefu wa mikono 28* na upana wa mikono 4. Vita-mbaa vyote vitakuwa na ukubwa uleule.^e **3** Vitambaa vitano vya hema la ibada vitaunganishwa pamoja na kuwa kitambaa kimoja kirefu, na vitambaa vile vingine vitano vitaunganishwa pamoja na kuwa kitambaa kimoja kirefu. **4** Utatengeneza vitanzi vya nyuzi za bluu kwenye upindo wa kitambaa cha mwisho, nawe utafanya vivyo hivyo kwenye upindo wa kitambaa kile kingine mahali ambapo vitaunganishwa. **5** Utatengeneza vitanzi 50 kwenye kitambaa kimoja na vitanzi vingine 50 kwenye upindo wa kitambaa cha pili ili vitanzi hivyo vielekeane vitakapounganishwa. **6** Nawe utatengeneza vibanio 50 vya dhahabu na kuunganisha vitambaa hivyo pamoja kwa vibanio hivyo, ili

25:39 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. 25:40 *Au “mchoro ulioonyeshwa.” 26:2 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 25

a Kut 39:42
Hes 8:4
Mdo 7:44
Ebr 8:5

SURA YA 26

b Ebr 8:5
Ebr 9:9,11

c Mwa 3:24
Zb 99:1

d Kut 36:8-13

e Hes 4:25

Safu ya 2

a Kut 39:33,34

b Kut 35:26

c Kut 36:14-18

d Kut 36:19

e Hes 4:29,31

f Kut 36:20-23

hema la ibada liwe na kitambaa kimoja kizima.^a

7 “Pia utatengeneza vitambaa vya manyoya ya mbuzi^b vya kufunika hema hilo. Utatengeneza vitambaa 11 vya hema.^c **8** Kila kitambaa kita-kuwa na urefu wa mikono 30 na upana wa mikono 4. Vitambaa vyote 11 vitakuwa na ukubwa uleule. **9** Utaunganisha vitambaa vitano pamoja na kitambaa cha sita utakikunja upande wa mbele wa hema. **10** Kisha utatengeneza vitanzi 50 kwenye upindo wa kitambaa cha kwanza, kwenye kipande cha mwisho kabisa, na vitanzi 50 kwenye upindo wa kitambaa cha pili, mahali vita-kapounganishwa. **11** Nawe utatengeneza vibanio 50 vya shaba na kuvitia kwenye vitanzi na kuunganisha vitambaa hivyo pamoja, ili hema liwe na kitambaa kimoja kizima. **12** Sehemu inayobaki ya vitambaa vya hema itaning’inia. Nusu inayobaki ya kitambaa cha hema itaning’inia upande wa nyuma wa hema. **13** Sehemu inayobaki ya vitambaa hivyo itaning’inia pande zote za hema kwa urefu wa mkono mmoja kila upande, ili kulifunika hema.

14 “Utatengeneza pia kifuniko kingine cha hema kwa kutumia ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu na juu yake kifuniko cha ngozi za sili.^d

15 “Utatengeneza viunzi vya mbao^e za mshita vilivyo wima kwa ajili ya hema hilo.^f

16 Kila kiunzi kitakuwa na urefu wa mikono kumi na upana wa mkono mmoja na nusu.

17 Kila kiunzi kitakuwa na ndimi mbili* zilizounganishwa pamoja. Hivyo ndivyo utakavyotengeneza viunzi vyote vya hema la ibada. **18** Utatengeneza viunzi 20 kwa ajili ya upande wa kusini wa hema la ibada.

19 "Utatengeneza vikalio 40 vya fedha^a chini ya vile viunzi 20: vikalio viwili chini ya kiunzi kimoja pamoja na ndimi zake mbili, na vikalio viwili chini ya kila kiunzi kinachofuata pamoja na ndimi zake mbili.^b **20** Utatengeneza viunzi 20 upande wa pili wa hema, upande wa kaskazini **21** pamoja na vikalio vyake 40 vya fedha, vikalio viwili chini ya kiunzi kimoja na vikalio viwili chini ya kila kiunzi kinachofuata. **22** Utatengeneza viunzi sita sehemu ya nyuma ya hema la ibada, upande wa magharibi.^c **23** Nawe utatengeneza viunzi viwili viwe mihimili miwili ya pembeni upande wa nyuma wa hema la ibada. **24** Katika pembe zote mbili kutakuwa na viunzi viwili kuanzia sehemu ya chini mpaka sehemu ya juu, kwenye pete ya kwanza. Hivyo ndivyo utakavyotengeneza viunzi vyote viwili; vitakuwa mihimili miwili ya pembeni. **25** Kutakuwa na viunzi vinane na vikalio vyake 16 vya fedha, vikalio viwili chini ya kiunzi kimoja na vikalio viwili chini ya kila kiunzi kinachofuata.

26 "Utatengeneza fito za mshita, fito tano kwa ajili ya viunzi vya upande mmoja wa hema la ibada,^d **27** na fito tano kwa ajili ya viunzi vya

SURA YA 26

a Hes 3:36

b Kut 36:24-26

c Kut 36:27-30

d Kut 36:31-33

Safu ya 2

a Kut 12:35, 36
Kut 36:34b Kut 19:3
Kut 25:9
Mdo 7:44
Ebr 8:5c Kut 36:35, 36
Lu 23:45
Ebr 6:19
Ebr 9:3
Ebr 10:19, 20

d 1Fa 8:6

e Kut 40:22, 26

f Kut 40:21
Law 16:2
1Fa 8:6
Ebr 9:2-4
Ebr 9:12, 24g Law 24:2, 3
1Fa 7:48, 49

h Kut 36:37, 38

upande wa pili wa hema la ibada, na fito tano kwa ajili ya viunzi vya sehemu ya nyuma wa hema la ibada, upande wa magharibi. **28** Ufito ulio katikati ya viunzi utatoka mwisho mmoja mpaka mwingine.

29 "Nawe utavifunika viunzi hivyo kwa dhahabu^e na kutengeneza pete za dhahabu ili zishikilie fito, na fito hizo utazifunika kwa dhahabu. **30** Utatengeneza hema la ibada kwa kufuata ramani ambayo nilikupa mlimani.^b

31 "Utatengeneza pazia^c la nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nye-kundu, na kitani bora kilichosokotwa. Utalitarizi kwa michoro ya makerubi. **32** Utalining'iniza kwenye nguzo nne za mshita zilizofunikwa kwa dhahabu. Kulabu zake zitakuwa za dhahabu. Nguzo hizo zitakaa juu ya vikalio vinne vya fedha. **33** Utalining'iniza pazia hilo chini ya vibanio na kuleta sanduku la Ushahidi^d humo, nyuma ya pazia. Pazia hilo litatenganisha Patakatifu^e na Patakatifu Zaidi.^f **34** Utaweka kile kifuniko juu ya sanduku la Ushahidi ndani ya Patakatifu Zaidi.

35 "Utaiweka ile meza nje ya pazia, na kinara cha taa^g kitaelekeana na meza hiyo upande wa kusini wa hema la ibada; utaiweka meza upande wa kaskazini. **36** Kwa ajili ya mlango wa hema, utatengeneza pazia la nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa na kufumwa.^h **37** Utatengeneza nguzo tano za mshita na kuzifunika kwa dhahabu kwa ajili ya

pazia hilo. Kulabu zake zitakuwa za dhahabu, nawe utazitengenezea vikatio vitano vya shaba.

27 "Utatengeneza madhabahu kwa mbao za mshita;^a itakuwa na urefu wa mikono mitano* na upana wa mikono mitano. Madhabahu hiyo itakuwa ya mraba na kimo chake kitakuwa mikono mitatu.^b **2** Utatengeneza pembe^c kwenye ncha zake nne; pembe hizo zitakuwa sehemu ya madhabahu, nawe utafunika madhabahu hiyo kwa shaba.^d **3** Utatengeneza ndoo za kuondolea majivu,* pia sepetu, mabakuli, nyuma,^e na vyetezo; utatengeneza vyombo vyote vya madhabahu kwa shaba.^e **4** Nawe utatengeneza wavu wa shaba kwa ajili ya madhabahu, pia utatengeneza pete nne za shaba kwenye pembe nne za wavu huo. **5** Nawe utauweka wavu huo chini ya ukingo wa madhabahu, nao utashuka ndani ya madhabahu kufikia katikati. **6** Utatengeneza fito za mshita kwa ajili ya madhabahu na kuzifunika kwa shaba. **7** Fito hizo zitaingizwa kwenye zile pete ili ziwe katika pande mbili za madhabahu wakati inapobebwa.^f **8** Utatengeneza madhabahu hiyo kama sanduku la mbao lenye uwazi. Inapaswa kutengenezwa kama tu Alivyokuonyesha mlimani.^g

9 "Utatengeneza ua wa hema^h la ibada. Upande wa

27:1 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. 27:3 *Au "majivu yenye mafuta," yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhabihu. ^eWingi wa kifaa kinachoitwa uma.

SURA YA 27

a Kut 40:29
2Nya 4:1
Ebr 13:10

b Kut 38:1-7

c Law 4:25

d 1Fa 8:64

e 1Fa 7:45

f Hes 4:14,15

g Kut 25:40
1Nya 28:12
Mdo 7:44
Ebr 8:5

h Kut 40:8
1Fa 6:36

Safu ya 2

a Kut 38:9-15

b Kut 39:33,40

c Kut 35:25

d Kut 38:18,19

e Kut 38:17

kusini, ua huo utakuwa na mapazia yanayoning'inia ya kitani bora kilichosokotwa; yatakuwa na urefu wa mikono 100 upande mmoja.^a **10** Ua huo utakuwa na nguzo 20 na vikatio 20 vya shaba. Kulabu za nguzo hizo pamoja na vitanzi* vyake vitakuwa vya fedha. **11** Mapazia yanayoning'inia upande wa kaskazini yatakuwa pia na urefu wa mikono 100, pamoja na nguzo zake 20 na vikatio vyake 20 vya shaba, lakini kulabu za nguzo hizo na vitanzi* vyake vitakuwa vya fedha. **12** Upande wa magharibi wa ua utakuwa na mapazia yanayoning'inia yenye urefu wa mikono 50, na nguzo 10 na vikatio 10. **13** Ua utakuwa na upana wa mikono 50 upande wa mashariki, yaani, upande wa mapambazuko ya jua. **14** Mapazia yanayoning'inia yenye upana wa mikono 15 yatakuwa upande mmoja, pamoja na nguzo tatu na vikatio vitatu.^b **15** Upande wa pili utakuwa na mapazia yanayoning'inia yenye upana wa mikono 15, pamoja na nguzo tatu na vikatio vitatu.

16 "Mlango wa ua utakuwa na pazia lenye urefu wa mikono 20 lililotengenezwa kwa nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa na kufumwa,^c pamoja na nguzo nne na vikatio vyake vinne.^d **17** Nguzo zote zinazozunguka ua zitakuwa na kulabu na vitanzi vya fedha, lakini vikatio vyake vitakuwa vya shaba.^e

27:10, 11 *Au "pete; vitanzi; vibanio" vya kushikia.

18 Ua huo utakuwa na urefu wa mikono 100,^a upana wa mikono 5, nao utatengenezwa kwa kitani bora kilichosokotwa, na utakuwa na vikalio vya shaba. **19** Vyombo na vitu vyote vitakavyotumiwa katika utumishi wa hema la ibada, pamoja na vingi vyote vya hema na vya ua, vitakuwa vya shaba.^b

20 “Utawaamuru Waisraeli wakuletee mafuta safi ya zeituni zilizopondwa ili taa ziwa-ke daima.^c **21** Katika hema la mkutano, nje ya pazia lili-lo karibu na sanduku la Ushahidi,^d Haruni na wanawe watahakikisha kwamba taa hizo zinawaka kuanzia jioni mpa-ka asubuhi mbele za Yehova.^e Hiyo ni sheria ya kudumu ka-tika vizazi vyao vyote itakayo-tekelezwa na Waisraeli.^f

28 “Utamleta Haruni^g ndu-gu yako pamoja na wa-nawe,^h Nadabu na Abihu,ⁱ Elezari na Ithamari^j kutoka miongoni mwa Waisraeli ili wanitumikie^k wakiwa maku-hani. **2** Utamtengenezea Ha-runi ndugu yako mavazi ma-takatifu ili awe na utukufu na fahari.^l **3** Waambie mafundi wote wenye ustadi,^m ambao nimewajaza roho ya hekima,ⁿ wamtengenezee Haruni mava-zi ili kumtakasa, ili anitumikie akiwa kuhani.

4 “Haya ndiyo mavazi wata-kayotengeneza: kifuko cha ki-fuani,ⁿ efodi,^o joho lisilo na mikono,^p kanzu yenye miraba, kilemba,^q na ukumbuu;^r wata-mtengenezea Haruni na wa-nawe mavazi haya matakati-fu ili wanitumikie wakiwa ma-

SURA YA 27

a Kut 27:9

b Kut 38:20
Hes 3:36, 37c Kut 39:33, 37
Law 24:1-3d Kut 26:33
Kut 40:3
Ebr 9:2, 3

e Kut 30:8

f Hes 18:23

SURA YA 28

g Ebr 5:4

h Kut 6:23
INya 6:3i Law 10:1
Hes 26:61j Kut 38:21
Law 10:16
INya 24:2k Law 8:2
Ebr 5:1l Kut 29:5
Law 8:7m Kut 31:6
Kut 36:1n Kut 39:8, 15
Law 8:8

o Kut 39:2

p Kut 39:22

q Kut 39:27, 28
Kut 39:30, 31
Law 8:9r Kut 39:27, 29
Law 8:7

Safu ya 2

a Kut 39:2-5

b Kut 29:5

c Kut 35:5, 9
Kut 35:27

d Kut 1:1-4

e Kut 39:6, 14

f Kut 39:7

g Kut 39:15

kuhani. **5** Mafundi hao stadi watatumia dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora.

6 “Watatengeneza efodi kwa dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya rangi ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa, nacho kinapaswa kutariziwa.^a **7** Efodi itakuwa na vipande viwili vya mabegani vitakavyounganishwa kwenye miisho yake miwili ya juu. **8** Mshipi uliofumwa^b unaoshikilia kwa nguvu efodi unapapasa kutengenezwa kwa vitu hivyo hivyo, yaani, dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya rangi ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa.

9 “Utachukua mawe mawili ya shohamu^c na kuchonga juu yake majina ya wana wa Israeli,^d **10** majina sita juu ya jiwe moja na majina mengine sita juu ya jiwe lingine, kulingana na umri wao. **11** Mchonga mawe atachonga majina ya wana wa Israeli kwenye mawe hayo mawili kama mtu anavyochonga muhuri.^e Kisha mawe hayo yatiwa katika vifuko vya dhahabu. **12** Utayaweka mawe hayo mawili kwenye vipande vya mabegani vya efodi, nayo yatakuwa mawe ya ukumbusho kwa wana wa Israeli,^f naye Haruni atayabeba majina yao kwenye vipande viwili vya efodi mabegani mwake kama ukumbusho mbele za Yehova. **13** Utatengeneza vifuko vya dhahabu **14** na minyororo miwili ya dhahabu safi iliyo-sokotwa kama kamba,^g utai-

fungu minyororo hiyo kwenye vifuko hivyo.^a

15 “Utamwagiza fundi wa kutarizi atengeneze kifuko cha kifuani cha maamuzi.^b Atakitengeneza kama efodi, kwa kutumia dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa.^c **16** Kifuko hicho kinapaswa kuwa cha mraba kinapokunjwa mara mbili, urefu wake uwe shubiri moja* na upana wake shubiri moja. **17** Unapaswa kuweka kwenye kifuko hicho mawe yaliyopangwa katika safu nne. Safu ya kwanza itakuwa na zbarijadi, topazi, na zumaridi. **18** Safu ya pili itakuwa na feruzi, yakuti, na yaspi. **19** Safu ya tatu itakuwa na jiwe la *leshemi*,* akiki, na amethysti. **20** Safu ya nne itakuwa na krisolito, shohamu, na yashefi. Mawe hayo yataweka kwenye vifuko vya dhahabu. **21** Mawe hayo yatalingana na majina 12 ya wana wa Israeli. Kila jina linapaswa kuchongwa kama muhuri unavyochongwa, na kila jina litawakilisha mojawapo ya makabila 12 ya wana wa Israeli.

22 “Utakitengenezea kifuko cha kifuani minyororo iliyosokotwa, kama kamba za dhahabu safi.^d **23** Pia utakitengenezea pete mbili za dhahabu na kuzitia kwenye pembe mbili za juu za kifuko hicho. **24** Utatia zile ka-

28:16 *Yaani, upana wa kiganja cha mkono kuanzia kidole gumba hadi kidole kidogo, karibu sentimita 22.2 (inchi 8.75). Angalia Nyongeza B14. **28:19** * Jiwe la thamani ambalo jina lake halijatajwa, huenda ni jiwe la kharabu, hayasinthi, opali, au tumalini.

SURA YA 28

a Kut 39:18

b Kut 28:30
Law 8:8
Hes 27:21

c Kut 39:8-14

d Kut 39:15-18

Safu ya 2

a Kut 39:19-21

b Kut 28:8
Law 8:7

c Law 8:8
Hes 27:21
Kum 33:8
1Sa 28:6
Ezr 2:62, 63

d Kut 39:22-26
Law 8:7

mba mbili za dhahabu katika pete mbili zilizo kwenye pembe za kifuko cha kifuani. **25** Kisha utatia ncha mbili za zile kamba mbili katika vile vifuko viwili vya mabegani, nawe unapaswa kuzifunga ncha hizo kwenye vipande viwili vya efodi, sehemu ya mbele. **26** Utatengeneza pete mbili za dhahabu na kuziweka kwenye pembe mbili za chini, upande wa ndani wa kifuko cha kifuani, upande wa efodi.^a **27** Utatengeneza pete nyingine mbili za dhahabu upande wa mbele wa efodi, chini ya vipande viwili vya mabegani vya efodi, karibu na mahali inapoungana, juu ya mshipi uliofumwa wa efodi.^b **28** Pete za kifuko cha kifuani zitafungwa pamoja na pete za efodi kwa kamba ya bluu. Hivyo, kifuko cha kifuani kitabaki mahali pake kwenye efodi, juu ya mshipi uliofumwa.

29 “Haruni atayabeba majina ya wana wa Israeli juu ya moyo wake kwenye kile kifuko cha kifuani cha maamuzi anapointa Patakatifu kama ukumbusho wa daima mbele za Yehova. **30** Utaweka Urimu na Thumimu*^c ndani ya kifuko cha kifuani cha maamuzi, nazo zitakuwa juu ya moyo wa Haruni anapointa mbele za Yehova, naye Haruni atabeba daima juu ya moyo wake vitu hivyo vya kufanyia maamuzi kwa ajili ya Waisraeli mbele za Yehova.

31 “Utatengeneza joho lisi- lo na mikono la efodi kwa nyuzi za bluu peke yake.^d **32** Litakuwa na nafasi ya kupitishia kichwa katikati upande

28:30 * Angalia Kamusi, uku. 2012.

wa juu. Sehemu hiyo itakuwa na ukingo uliofumwa kuingunguka. Itakuwa na ukingo kama wa koti la vita ili isiraruke. **33** Kwenye upindo wake wote, utatengeneza makomamanga ya nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kutia kengele za dhahabu katikati ya makomamanga. **34** Uta-tia kengele ya dhahabu kisha komamanga, kengele ya dhahabu kisha komamanga, kwenye upindo wote wa joho hilo lisilo na mikono. **35** Ni lazima Haruni alivae anapohudumu, na sauti ya kengele hizo inapaswa kusikika anapoingia patakatifu mbele za Yehova na anapotoka nje, ili asife.^a

36 "Utatengeneza bamba linalong'aa la dhahabu safi na kuchonga maneno haya juu kache kama muhuri unavyochongwa: 'Utakatifu ni wa Yehova.'^b **37** Ni lazima ulifunge bamba hilo kwenye kilemba^c kwa kamba ya bluu; litakuwa daima upande wa mbele wa kilemba. **38** Nalo litakuwa kwenye paji la uso wa Haruni, naye Haruni atawajibika Mwisraeli anapotenda kosa dhidi ya vitu vitakatifu^d vinavyotakaswa na Waisraeli wakati wanapovitoa kuwa zawadi takatifu. Ni lazima bamba hilo likae sikuzote kwenye paji la uso wake, ili wapate kibali mbele za Yehova.

39 "Utafuma kanzu ya kitani bora yenye miraba, utatengeneza kilemba cha kitani bora, na kufuma ukumbuu.^e

40 "Pia utawatengeneza wana wa Haruni kanzu,^f ukumbuu, na kofia, ili wawe na utukufu na fahari.^g **41** Utamvisha Haruni ndugu yako na

SURA YA 28

a Law 16:2
Hes 18:7

b Kut 39:30, 31
Law 8:9
1Nya 16:29
Zb 93:5
1Pe 1:16

c Kut 29:6

d Law 22:9
Hes 18:1

e Kut 28:4
Kut 39:27-29

f Law 8:13

g Kut 28:2

Safu ya 2

a Kut 29:4, 7
Kut 30:30
Mdo 10:38
2Ko 1:21

b Kut 29:8, 9
Law 8:33
Hes 3:2, 3

c Law 6:10

SURA YA 29

d Law 8:2
Kum 17:1

e Law 6:20

f Law 8:26

g Kut 26:36
Kut 40:28
Law 8:2, 3

h Law 8:6
Ebr 10:22

i Kut 28:4
Law 8:7
Law 16:4

j Kut 28:8

wanawe mavazi hayo, nawe utawatia mafuta^a na kuwaweka rasmi^{*b} na kuwatakasasa, nao watanitumikia wakiwa makuhani. **42** Pia watengenezee suruali fupi* za kitani ili kufunika uchi wao.^c Suruali hizo zitawafunika kuanzia kiunoni mpaka mapajani. **43** Haruni na wanawe wataziva wanapoingia kwenye hema la mkutano au wanapokaribia madhabahu kuhudumu mahali patakatifu, ili wasipatwe na hatia na kufa. Ni sheria ya kudumu kwa Haruni na uzao wake.*

29 "Hivi ndivyo utakavyo watakasasa ili wanitumikie wakiwa makuhani: Chukua ng'ombe dume mchanga, kondoo dume wawili wasio na kasoro,^d **2** mikate isiyo na chachu, mikate ya mviringo isiyo na chachu na iliyo-kandwa kwa mafuta, na mikate myembamba isiyo na chachu na ambayo imepakwa mafuta.^e Utaioka kwa unga laini wa ngano **3** na kuiweka ndani ya kikapu, nawe utaiteta mbele zangu ikiwa ndani ya kikapu,^f pamoja na yule ng'ombe dume na wale kondoo dume wawili.

4 "Utamleta Haruni na wanawe kwenye mlango wa hema la mkutano^g na kuwao-sha kwa maji.^h **5** Kisha utachukua yale mavaziⁱ na kumvisha Haruni kanzu, joho la efodi lisilo na mikono, efodi, na kifuko cha kifuani, nawe utamfunga vizuri kabisa kiunoni ule mshipi uliofumwa wa efodi.^j **6** Utamvisha kile kile-

28:41 *Tnn., "na kuijaza mikono yao."
28:42 *Au "nguo za ndani." 28:43
*Tnn., "mbegu yake."

mba kichwani na kuiweka ile ishara takatifu ya wakfu* kwenye kilemba hicho;^a **7** kisha chukua mafuta yanayotumiwa kutia mafuta^b na uyamimine juu ya kichwa chake na kumtia mafuta.^c

8 "Halafu walete wanawe na kuwavisha kanzu^d **9** na umfungue Haruni na wanawe ukumbuu viunoni na kuwavisha kofia zao; ukuhani utakuwa wao, nayo itakuwa sheria ya kudumu.^e Hivyo ndivyo utakavyowaweka rasmi Haruni na wanawe ili watumike wakiwa makuhani.^{*f}

10 "Sasa utamleta yule ng'ombe dume mbele ya hema la mkutano, na Haruni na wanawe wataweka mikono yao juu ya kichwa cha huyo ng'ombe dume.^g **11** Mchinje huyo ng'ombe dume mbele za Yehova, kwenye mlango wa hema la mkutano.^h **12** Chukua kiasi fulani cha damu ya huyo ng'ombe dume kwa kidole chako na kuitia kwenye pembe za madhabahu,ⁱ kisha umwage damu yote inayobaki chini kwenye msingi wa madhabahu.^j **13** Kisha chukua mafuta yote^k yanayofunika matumbo, mafuta yaliyo juu ya ini, na figo zake mbili na mafuta yaliyo juu yake, nawe uchome moto vitu hivyo ili vifuke moshi juu ya madhabahu.^l **14** Lakini nyama ya ng'ombe dume huyo na ngozi yake na mavi yake utavitekeza nje ya kambi. Hiyo ni dhambi ya dhambi.

15 "Kisha utamchukua kondoo dume mmoja, naye Ha-

29:6 *Au "lile taji takatifu." **29:9** *Tnn., "Hivyo ndivyo utakavyoujaza mkono wa Haruni na mikono ya wanawe."

SURA YA 29

a Kut 28:36
Kut 39:30
Law 8:9

b Kut 30:23-25

c Law 8:12
Zb 133:2
Isa 61:1
Mdo 10:38

d Kut 28:40
Law 8:13

e Kut 28:1-3
Kut 28:40, 43
Kut 40:15

f Kut 28:41

g Law 8:14-17

h Law 4:3

i Kut 27:2

j Law 4:7

k Law 3:17

l Law 4:8-10

Safu ya 2

a Law 1:4
Law 8:18-21

b Ebr 9:22

c Law 1:13

d Mwa 8:21

e Law 8:22-24

f Kut 30:23-25

g Law 8:30

runi na wanawe wataweka mikono yao juu ya kichwa cha huyo kondoo dume.^a **16** Mchinje kondoo dume huyo, uchukue damu yake na kuinunyiza pande zote za madhabahu.^b **17** Mkatete kondoo dume huyo vipandevipande, uoshe matumbo yake^c na miguu yake, na kuvipanga vipande hivyo pamoja na kichwa chake. **18** Utamchoma moto huyo kondoo mzima ili afuke moshi juu ya madhabahu. Ni dhambi ya kuteketewa kwa Yehova, harufu inayompendeza.^{*d} Ni dhambi kwa Yehova inayochomwa kwa moto.

19 "Kisha utamchukua kondoo dume wa pili, na Haruni na wanawe wataweka mikono yao juu ya kichwa cha kondoo huyo.^e **20** Mchinje kondoo dume huyo na uchukue kiasi fulani cha damu yake na kuitia kwenye ncha ya sikio la kulia la Haruni na kwenye ncha za masikio ya kulia ya wanawe na kwenye vidole gumba vya mikono yao ya kulia na kwenye vidole gumba vya miguu yao ya kulia, nawe unyunyize damu pande zote za madhabahu. **21** Kisha chukua kiasi fulani cha damu iliyo kwenye madhabahu na baadhi ya mafuta yanayotumiwa kutia mafuta,^f nawe umnyunyizie Haruni na mavazi yake na wanawe na mavazi yao, ili awe mtakatifu yeye na mavazi yake na wanawe na mavazi yao.^g

22 "Halafu chukua mafuta ya huyo kondoo dume, mkia wake mnono, mafuta yanayofunika matumbo, mafuta

29:18 *Au "inayomtuliza."

yaliyo juu ya ini, figo zake mbili na mafuta yaliyo juu yake,^a na mguu wa kulia, kwa maana huyo ni kondoo dume wa kumweka rasmi kuhani.^b **23** Chukua pia mkate wa miringo na mkate wa miringo uliokandwa kwa mafuta na mkate mwembamba kutoka katika kile kikapu cha mikate isiyo na chachu kilicho mbele za Yehova. **24** Ni lazima uviweke vitu hivyo vyote mikononi mwa Haruni na mikononi mwa wanawe, nawe utavitikisa kwenda mbele na nyuma vikiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova. **25** Kisha utavichukua vitu hivyo kutoka mikononi mwao na kuvitekeza juu ya madhabahu, juu ya dhabihu ya kutekelezwa, ili viwe harufu inayompendeza* Yehova. Ni dhabihu kwa Yehova inayochoywa kwa moto.

26 "Halafu chukua kidari cha kondoo dume wa kumweka rasmi kuhani,^c anayetolewa kwa ajili ya Haruni, nawe ukitikise kwenda mbele na nyuma kikiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova, nacho kitakuwa fungu lako. **27** Utakitakasa kidari cha toleo la kutikiswa na ule mguu wa fungu takatifu ambao ulitikiswa na ambao ulichukuliwa kutoka kwa yule kondoo dume wa kumweka rasmi kuhani,^d aliyetolewa kwa ajili ya Haruni na wanawe. **28** Vitu hivyo vitakuwa vya Haruni na wanawe kulingana na sheria ya kudumu itakayotekelezwa na Waisraeli, kwa sababu vitu hivyo ni fungu takatifu, navyo vitakuwa fungu takatifu lita-

29:25 * Au "inayomtuliza."

SURA YA 29

a Law 3:9, 10

b Law 8:22
Law 8:25-28

c Law 8:29
Zb 99:6

d Kut 29:22

Safu ya 2

a Law 7:34
Law 10:14

b Law 7:11, 14

c Kut 28:4

d Hes 20:26

e Law 8:35

f Law 8:31

g Iko 9:13

h Law 22:10
Hes 3:10

i Law 8:32

j Law 8:4, 33

kalotolewa na Waisraeli.^a Ni fungu lao takatifu kwa Yehova kutoka katika dhabihu zao za ushirika.^b

29 "Mavazi matakatifu^c ya Haruni yatatumiwa na wanawe^d baada yake watakapotiwa mafuta na kuwekwa rasmi kuwa makuhani. **30** Mwanwa wa Haruni atakayewe kwa kuwa kuhani baada yake na ambaye ataingia katika hema la mkutano ili kuhudumu mahali patakatifu atayavaa mavazi hayo kwa siku saba.^e

31 "Utamchukua yule kondoo dume wa kumweka rasmi kuhani na kuichemshia nyama yake mahali patakatifu.^f

32 Haruni na wanawe wataila^g nyama ya kondoo dume huyo na mikate iliyo katika kikapu kwenye mlango wa hema la mkutano. **33** Watakula vitu vilivyotolewa dhabihu ili kufunika dhambi wakati walipowekwa rasmi kuwa makuhani* na kutakaswa. Lakini mtu ambaye hana idhini^h hapaswi kuvila, kwa maana ni vitakatifu.^h **34** Ikiwa nyama yoyote ya dhabihu ya kumweka rasmi kuhani na mkate wowote utabaki mpaka asubuhi, unapaswa kutekeleza kinachobaki.ⁱ Hakipaswi kuliwa kwa sababu ni kitakatifu.

35 "Hivi ndivyo utakavyomfanyia Haruni na wanawe, kulingana na yote niliyo kuamuru. Utatumia siku saba kuwaweka rasmi kuwa makuhani.*^j **36** Kila siku utamtoa ng'ombe dume wa dhabihu ya

29:33 * Tnn., "ili kuijaza mikono yao." ^a Tnn., "mgeni," yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni. 29:35 * Tnn., "kuijaza mikono yao."

dhambi ili kufunika dhambi zao, nawe utaitakasa madhabahu kwa kutoa dhabihu ya kufunika dhambi ya madhabahu hiyo, nawe utaitia mafuta ili kuitakasa.^a **37** Utatumia siku saba kufunika dhambi ya madhabahu, nawe lazima uitakase ili iwe madhabahu takatifu kabisa.^b Mtu yeye anayeigusa madhabahu hiyo anapaswa kuwa mtaakatifu.

38 "Hivi ndivyo vitu utakavyotoa kwenye madhabahu: kila siku, kwa kuendelea,^c utatoa wanakondoo dume wawili wenye umri wa mwaka mmoja. **39** Mtoe mwanakondoo dume mmoja asubuhi na yule mwingine jioni kabla ya giza kuingia.^{*d} **40** Sehemu ya kumi ya kipimo cha efa moja* ya unga laini uliochanganywa na robo ya hini[#] ya mafuta ya zeituni zilizopondwa, na toleo la kinywaji la robo ya hini ya divai, vitatolewa pamoja na mwanakondoo dume wa kwanza. **41** Utamtoa mwanakondoo dume wa pili jioni kabla ya giza kuingia,* pamoja na matoleo ya nafaka na kinywaji kama yale ya asubuhi. Utamtoa akiwa harufu inayopendeza,[#] dhabihu kwa Yehova inayochomwa kwa moto. **42** Itakuwa dhabihu ya kuteketezwa itakayotolewa kwa ukawaida katika vizazi vye nu vyote kwenye mlango wa hema la mkutano mbele za Yehova, mahali ambapo nitawatokea ili kuzungumza nanyi.^e

29:39, 41 *Tnn., "katikati ya zile jioni mbili." **29:40** *Efa ilikuwa sawa na lita 22 au kilogramu 13 hivi. Angalia Nyongeza B14. [#]Hini ilikuwa sawa na lita 3.67. Angalia Nyongeza B14. **29:41** *Au "inayotuliza."

SURA YA 29

a Kut 30:26, 28
Law 8:11
Hes 7:1

b Kut 40:10

c 2Nya 2:4
Ebr 7:27
Ebr 10:11

d Hes 28:4-6

e Kut 25:22
Law 1:1
Hes 17:4

Safu ya 2

a Kut 40:34
Hes 12:5
IFa 8:11

b Law 22:9

c Kut 25:8
Law 26:12
Zek 2:11
2Ko 6:16

d Kut 20:2

SURA YA 30

e Kut 40:5

f Kut 37:25-28

g Kut 27:1, 2
Law 4:7

h Kut 26:33
Ebr 9:3

i Kut 25:22

j 1Nya 23:13

k Kut 30:34, 35

43 "Hapo ndipo nitakapowatokea Waisraeli, na utukuwangu utapatakasa mahali hapo.^a **44** Nitalitakasa hema la mkutano na madhabahu, nami nitamtakasa Haruni na wanawe^b ili wanitumikie wakiwa makuhani. **45** Nitakaa* miongoni mwa Waisraeli, nami nitakuwa Mungu wao.^c **46** Nao hakika watajua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao, niliyewatoa katika nchi ya Misri ili nikae miongoni mwao.^d Mimi ni Yehova Mungu wao.

30 "Utajenga madhabahu ya kufukizia uvumba;^e utajenga kwa mbao za mshita.^f **2** Itakuwa ya mraba; urefu wa mkono mmoja,* upana wa mkono mmoja, na kimo cha mikono miwili. Pembe zake zitakuwa sehemu ya madhabahu hiyo.^g **3** Utaiifunika kwa dhahabu safi: sehemu yake ya juu, pande zote kuizunguka, na pembe zake; nawe utatengeneza ukingo wa dhahabu kuizunguka. **4** Pia, utaitengenezea pete mbili za dhahabu chini ya ukingo wake kwenye pande zake mbili zinazoelekeana, na pete hizo zitashikilia fito za kubebea madhabahu. **5** Tengeneza fito za mshita na kuzifunika kwa dhahabu. **6** Utaiweka mbele ya pazia lililo karibu na sanduku la Ushahidi,^h mbele ya kifuniko kilicho juu ya sanduku la Ushahidi, mahali nitakapokutokea.ⁱ

7 "Haruni^j atafukiza uvumba wenye manukato^k juu

29:45 *Au "Nitapiga hema." **30:2** *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

ya madhabahu hiyo^a kila asubuhi anaposhughulikia taa.^b **8** Pia, Haruni anapowasha taa jioni kabla ya giza kuingia,* atafukiza uvumba. Ni uvumba unaofukizwa kwa ukawaida mbele za Yehova katika viza-zi vyenu vyote. **9** Hampaswi kufukiza uvumba usio halali^c au kutoa juu yake dhabihu ya kuteketezwa au toleo la nafaka, wala hampaswi kumimina juu yake toleo la kinywaji. **10** Haruni anapaswa kutoa dhabihu ya kufunika dhambi juu ya pembe za madhabahu hiyo mara moja kwa mwaka.^d Akitumia kiasi fulani cha damu ya dhabihu ya dhambi inayotolewa ili kufunika dhambi,^e ataitakasa mara moja kwa mwaka katika viza-zi vyenu vyote. Ni madhabahu takatifu zaidi kwa Yehova.”

11 Kisha Yehova akamwambia Musa: **12** “Wakati wote unapowahesabu wana wa Israeli,^f ni lazima kila mmoja wao anipe mimi Yehova fidia kwa ajili ya nafsi yake* watu wanapohesabiwa. Watafanya hivyo ili wasipatwe na pigo lolote wanapoandikishwa. **13** Wote watakaandikishwa watatoa nusu ya shekeli* kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.”^g Gera 20^h ni sawa na shekeli moja. Nusu shekeli ni mchango kwa Yehova.^h **14** Kila mtu mwenye umri wa kuanzia miaka 20 anayeandiki-

30:8 *Tnn., “Katikati ya zile jioni mbili.” 30:12 *Au “uhai wake.” 30:13, 15 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. 30:13 *Au “shekeli takatifu.” ^aGera moja ilikuwa na uzito wa gramu 0.57. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 30

a Hes 16:39, 40
1Sa 2:27, 28
Lu 1:9

b Kut 27:20

c Law 10:1
2Nya 26:18
Eze 8:11, 12

d Law 23:27
Ebr 9:7

e Law 16:5, 6
Law 16:18, 19

f Kut 38:25
Hes 1:2
2Sa 24:10, 15

g Law 27:25

h 2Nya 24:9
Mt 17:24

Safu ya 2

a Kut 38:26
Hes 1:3
Hes 26:1, 2

b Kut 38:8
Law 8:11
1Fa 7:38

c Kut 40:7

d Kut 40:30, 31
Ebr 10:22

e 2Nya 4:6

kishwa atatoa mchango wa Yehova.^a **15** Tajiri hapaswi kutoa zaidi na maskini hapaswi kutoa mchango wa Yehova unaopungua nusu shekeli* ili kutoa dhabihu ya kufunika dhambi kwa ajili ya nafsi zenu.^b **16** Unapaswa kuchukua kutoka kwa Waisraeli fedha za dhabihu ya kufunika dhambi na kuzitoa ili zitumiwe katika utumishi wa hema la mkutano, ziwe kumbukumbu mbele za Yehova kwa ajili ya Waisraeli, ili kufunika dhambi kwa ajili ya nafsi zenu.”*

17 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **18** “Tenge neza beseni la kunawia la shaba pamoja na kinara chake;^b kisha uliweke kati ya hema la mkutano na madhabahu na utie maji ndani yake.^c **19** Haruni na wanawe watanawa mikono na miguu yao kwenye beseni hilo.^d **20** Wanapoingia kwenye hema la mkutano au wanapoenda kwenye madhabahu kuhudumu na kumtolea Yehova dhabihu za kuteketezwa na zinazofuka moshi, watanawa kwa maji ili wasife. **21** Ni lazima wanawe mikono na miguu ili wasife, nayo itakuwa sheria ya kudumu kwa ajili yao, yaani, kwa Haruni na uzao wake, katika vizazi vyao vyote.”^e

22 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **23** “Kisha, chukua manukato bora kabisa: kilogramu 6 za manemane iliyoganda, kilogramu 3 za mdalasini wenye harufu nzuri, kilogramu 3 za kane, **24** na kilogramu 6 za kida, zilizo-pimwa kwa shekeli ya kawai-

30:15 *Tnn., “kwa ajili ya uhai wenu.”
30:16 *Au “uhai wenu.”

da ya mahali patakatifu,*^a pamoja na hini moja[#] ya mafuta ya zeituni. **25** Kisha utumie manukato hayo kutengeneza mafuta matakatiifu ya kutia mafuta; manukato hayo ya napaswa kuchanganywa pamoja kwa ustadi.*^b Yatakuwa mafuta matakatiifu ya kutia mafuta.

26 "Utayatumia kutia mafuta hema la mkutano^c na sanduku la Ushahidi, **27** pamoja na meza na vyombo vyake vyote, kinara cha taa na vyombo vyake, madhabahu ya uvumba, **28** madhabahu ya dhabihu za kuteketewa na vyombo vyake vyote, na lile beseni pamoja na kinara chake. **29** Ni lazima uvitakase ili viwe vitakatiifu kabisa.^d Yeyote anayevigusa anapaswa kuwa mtakatiifu.^e **30** Nawe utamtia mafuta Haruni^f na wanawe^g na kuwatakasika ili wanitumikie wakiwa makuhani.^h

31 "Nawe utawaambia Waisraeli, 'Mafuta haya ya kutia mafuta yataendelea kuwa matakatiifu kwangu katika vizazi vyenu.ⁱ **32** Hayapaswi kupakwa kwenye ngozi ya mwanaadamu, nanyi hampaswi kutengeneza kitu chochote chenye mchanganyiko kama huo. Ni mafuta matakatiifu. Yataendelea kuwa matakatiifu kwenu. **33** Mtu yeyote anayetengeneza mafuta kama hayo na kumpaka mtu asiye na idhini* ni lazima auawe."^j

30:24 *Au "shekeli takatiifu." [#]Hini ilikuwa sawa na lita 3.67. Angalia Nyoengeza B14. **30:25, 35** *Au "kama anayofanya mtengenezaji wa manukato." **30:33** *Tnn., "mgeni," yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni.

SURA YA 30

a Hes 3:47

b Kut 37:29

c Kut 40:9
Hes 7:1

d Law 8:10

e Kut 29:37

f Law 8:12

g Hes 3:2, 3

h Kut 40:15

i Kut 37:29
1Fa 1:39
Zb 89:20

j Kut 30:37, 38

Safu ya 2

a Kut 25:3, 6

b Kut 37:29
Zb 141:2
Ufu 5:8

c Law 2:13

d Kut 30:31, 32

SURA YA 31

e Kut 37:1

f Kut 35:30-34
1Nya 2:20

g Kut 28:9-11

h 2Nya 2:13, 14

i Kut 38:23

j Kut 36:1

k Kut 36:8

l Kut 37:1

34 Kisha Yehova akamwambia Musa: "Chukua vipimo vinavyolingana vya manukato haya:^a matone ya natafi, shekelethi, kelbena yenye manukato, na ubani safi. **35** Yatumie kutengeneza uvumba;^b viungo hivyo vinapaswa kuchanganywa kwa ustadi,* vitiwe chumvi,^c viwe safi, na vitakatiifu. **36** Utaponda baadhi ya viungo hivyo viwe unga laini na kuweka kiasi fulani mbele ya sanduku la Ushahidi katika hema la mkutano, mahali nitakapokutokea. Mchanganyiko huo unapaswa kuwa mtakatiifu kabisa kwenu. **37** Hampaswi kutumia mchanganyiko huo kujitengeneza uvumba kwa ajili ya matumizi yenu.^d Mnapaswa kuuona kuwa mtakatiifu kwa Yehova. **38** Yeyote atakayetengeneza uvumba kama huo ili afurahie harufu yake ni lazima auawe."

31 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** "Tazama, nimemchagua* Bezaleli^e mwana wa Uri mwana wa Huru wa kabila la Yuda.^f **3** Nitamjaza roho ya Mungu, na kumpa hekima, uelewaji, na ujuzi katika kila aina ya ufundi, **4** ili abuni kazi za usanii akitumia dhahabu, fedha, na shaba, **5** ili achonge na kupamba kwa mawe,^g na kutengeneza vifaa vya mbao vya kila aina.^h **6** Pia, nimemchagua Oholiabuⁱ mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani ili amsaidie, nami ninaweka hekima katika mioyo ya wote wenye ustadi,* ili watengeneze kila kitu nilichokuamuru:^j **7** hema la mkutano,^k sanduku la Ushahidi^l na

31:2 *Tnn., "nimemwita kwa jina." **31:6** *Au "wenye hekima moyoni."

kifuniko chake,^a vyombo vyote vya hema, **8** meza^b na vyombo vyake, kinara cha taa cha dhahabu safi na vyombo vyake vyote,^c madhabahu ya uvumba,^d **9** madhabahu ya dhahabu za kuteketezwa^e na vyombo vyake vyote, beseni na kinara chake,^f **10** yale mavazi bora yaliyofumwa, mavazi matakatifu ya kuhani Haruni, mavazi ya wanawe ya kutumikia wakiwa makuhani,^g **11** mafuta yanayotumiwa kutia mafuta, na ule uvumba wenye manukato kwa ajili ya mahali patakatifu.^h Watafanya mambo yote niliyokuamuru.”

12 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **13** “Waaambia Waisraeli, ‘Mnapaswa hasa kushika sabato zangu,ⁱ kwa maana ni ishara kati yangu pamoja nanyi katika vizazi vyenu ili mjue kwamba mimi, Yehova, ninawatakasa ninyi. **14** Ni lazima mshike Sabato kwa sababu ni takatifu kwenu.^j Mtu yeyote atakayeitia unajisi ni lazima auawe. Mtu yeyote atakayefanya kazi siku hiyo, ni lazima auawe kutoka kati ya watu wake.^k **15** Mnaweza kufanya kazi kwa siku sita, lakini siku ya saba ni sabato ya pumziko kamili.^l Ni takatifu kwa Yehova. Mtu yeyote atakayefanya kazi siku ya Sabato ni lazima auawe. **16** Ni lazima Waisraeli washike Sabato; ni lazima waadhimisha Sabato katika vizazi vyao vyote. Ni agano la kudumu. **17** Ni ishara ya kudumu kati yangu na Waisraeli,^m kwa sababu katika siku sita mimi, Yehova, niliziumba mbingu na dunia na katika siku ya saba nilipumzika na kustarehe.”ⁿ

SURA YA 31

a Kut 37:6

b Kut 37:10

c Kut 37:17, 24

d Kut 37:25

e Kut 38:1
Kut 40:6f Kut 30:18
Kut 38:8g Kut 28:2, 15
Kut 39:1, 27
Law 8:7h Kut 30:25, 35
Kut 37:29i Kut 20:8
Law 19:30
Kol 2:16, 17

j Kum 5:12

k Kut 35:2
Hes 15:32, 35l Kut 16:23
Kut 20:10

m Kut 31:13

n Mwa 2:2

Safu ya 2

a Kut 24:12
Kut 32:15
Kum 4:13
Kum 9:15b Mt 12:28
Lu 11:20
2Ko 3:3

SURA YA 32

c Kut 24:18
Kum 9:9

d Mdo 7:40

e Kut 12:35, 36

f Kum 9:16
Isa 46:6
Mdo 7:41g Kut 20:4
Ne 9:18
Zb 106:19, 20

h 1Ko 10:7

18 Sasa mara tu alipomaliza kuzungumza naye kwenye Mlima Sinai, alimpa Musa mabamba mawili ya Ushahidi,^a mabamba ya mawe yaliyoandikwa kwa kidole cha Mungu.^b

32 Basi, watu wakaona kwamba Musa amekawia sana kushuka kutoka mlimani.^c Kwa hiyo wakakusanyika kumzunguka Haruni na kumwambia: “Haya, tutengenezee mungu atakayetuongoza^d kwa sababu hatuji liliimpa ta huyu Musa, mtu aliyetuongoza kutoka katika nchi ya Misri.” **2** Ndipo Haruni akawaambia: “Chukueni vipuli vya dhahabu^e ambavyo wake zenu, wana wenu, na binti zenu wamevaa masikioni mni-letee.” **3** Basi watu wote wakaanza kutoa vipuli vya dhahabu walivyokuwa wamevaa masikioni wakamletea Haruni. **4** Kisha akachukua dhahabu iliyokuwa kwenye vipuli hivyo, akatengeneza sanamu* ya ndama kwa kifaa cha kuchongea.^f Watu wakaanza kusema: “Huyu ndiye Mungu wenu, enyi Waisraeli, aliye-waongoza kutoka katika nchi ya Misri.”^g

5 Haruni alipoona hilo, akajenga madhabahu mbele ya sanamu hiyo na kutangaza hivi: “Kesho kutakuwa na sherehe kwa ajili ya Yehova.” **6** Basi wakaamka mapema siku iliyofuata na kuanza kutoa dhahabu za kuteketezwa na dhahabu za ushirika. Baada ya hayo watu wakaketi ili wale na kunywa. Kisha waka-simama ili wajitumbuize.^h

32:4 *Au “sanamu ya kuyeyushwa.”

7 Sasa Yehova akamwambia Musa: "Nenda, shuka, kwa sababu watu wako uliowaongoza kutoka katika nchi ya Misri wametenda uovu.*^a

8 Wamegeuka haraka na kua-cha njia niliyowaamuru wafuate.^b Wamejitengenezea sanamu* ya ndama, nao wanaendelea kuiinamia na kuitolea dhabihu wakisema, 'Huyu ndiye Mungu wenu, enyi Waisraeli, aliyewaongoza kutoka katika nchi ya Misri.'" 9 Yehova akaendelea kumwambia Musa: "Nimeona kwamba watu hawa ni wakaidi.*^c 10 Basi sasa, niache niwaangamize kabisa kwa hasira yangu inayowaka, na acha nikufanye wewe kuwa taifa kubwa."^d

11 Ndipo Musa akamsihi* Yehova Mungu wake^e akisema: "Ee Yehova, kwa nini uwaelekezee watu wako hasira yako inayowaka, baada ya kuwatoa katika nchi ya Misri kwa nguvu kuu na kwa mkono wenyewe nguvu?^f 12 Kwa nini Wamisri waseme, 'Alikuwa na nia ovu alipowatoa Misri. Alitaka kuwaua milimani na kuwaangamiza kabisa kutoka duniani?'^g Acha hasira yako inayowaka na ufikirie upya* uamuzi wako wa kuwaletea watu wako msiba huu. 13 Wakumbuke watumishi wako Abrahamu, Isaka, na Israeli, uliowaapia kwa jina lako mwenyewe na kusema, 'Nitaufanya uzao wenu uwe mwingi kama nyota za mbinguni,^h nami nitaupa uzao* wenu nchi yote

32:7 *Au "wamejichafua." 32:8 *Au "sanamu ya kuyeyushwa." 32:9 *Tnn., "wana shingo ngumu." 32:11 *Tnn., "akautuliza uso wa." 32:12 *Au "ughairi kuhusu." 32:13 *Tnn., "mbevu."

SURA YA 32

a Kum 4:15-18

b Kut 18:20
Kut 20:3c Kut 34:9
Kum 9:6
Mdo 7:51d Hes 14:12
Kum 9:14

e Zb 106:23

f Kum 9:18, 19

g Kum 9:28

h Mwa 22:15-17
Mwa 35:10, 11
Ebr 6:13, 14

Safu ya 2

a Mwa 13:14, 15
Mwa 26:3, 4

b Zb 106:45

c Kut 40:20
Kum 5:22

d Kum 9:15

e Kut 31:18
Kum 9:10f Ne 9:18
Zb 106:19, 20
Mdo 7:41

g Kum 9:16, 17

h Kum 7:25

i Kum 9:21

hii niliyowaahidi, ili iwe miliki yao ya kudumu."^a

14 Basi Yehova akaanza kufikiria upya* msiba ambao alikuwa amesema atawaletea watu wake.^b

15 Kisha Musa akageuka na kushuka kutoka mlimani akiwa amebeba yale mabamba mawili ya Ushahidi^c mikononi mwake.^d Mabamba hayo yalikuwa yameandikwa pande zote mbili; upande wa mbele na wa nyuma.

16 Mabamba hayo yalitengenezwa na Mungu, na maandishi yake yalikuwa maandishi ya Mungu yaliyochongwa kwenye mabamba hayo.^e 17 Yohua alipoanza kusikia sauti za watu wakipiga kelele, akamwambia Musa: "Kuna kelele za vita kambini." 18 Laki-ni Musa akasema:

"Si sauti za watu wanaoimba kwa sababu ya ushindi,*

Wala si sauti za watu wanaolia kwa sababu ya kushindwa;

Ninasikia sauti za uimbaji wa aina nyingine."

19 Mara tu Musa alipoikaribia kambi na kuona ile sanamu ya ndama^f na watu waki-cheza dansi, akaanza kuwaka hasira, naye akayatupa chini yale mabamba mawili yaliyokuwa mikononi mwake, yakavunjika-vunjika chini ya mlima.^g 20 Akaichukua sanamu ya ndama waliyokuwa wametengeneza, akaiteketeza na kuipondaponda ikawa ungaunga;^h kisha akaunyuni-za juu ya maji na kuwalazimisha Waisraeli wayanywe.ⁱ

32:14 *Au "kughairi kuhusu." 32:18 *Au "tendo la kishujaa."

21 Musa akamuuliza Haruni: “Watu hawa walikufanya nini hivi kwamba ukasababisha watende dhambi kubwa hivi?”

22 Haruni akajibu: “Usikasirike, bwana wangu. Unajua vizuri kwamba watu hawa wana mwelekeo wa kutenda mao-vu.^a **23** Basi waliniambia, ‘Tutengenezee mungu atakayetuongoza, kwa sababu hatujui lililompata huyu Musa, mtu aliyetuongoza kutoka katika nchi ya Misri.’^b **24** Basi nika-waambia, ‘Mtu yeyote aliye na dhahabu aitoe na kunipa.’ Kisha nikaitupa motoni na ndama huyu akatokea.”

25 Musa akaona kwamba watu wanafanya watakavyo, kwa sababu Haruni aliwaacha wafanye watakavyo, hivi kwamba wakajiletea aibu mbele ya wapinzani wao. **26** Kisha Musa akasimama kwenye lango la kambi na kusema: “Ni nani aliye upande wa Yehova? Njooi kwangu!”^c Ndipo Walawi wote wakakusanyika kumzunguka. **27** Basi Musa akawaambia: “Yehova Mungu wa Israeli amesema, ‘Kila mmoja wenu na ajifunge upanga wake na kupita kotekote kambini, kutoka lango mpaka lango, amuue ndugu yake, jirani yake, na rafiki yake wa karibu.’”^d **28** Walawi wakafanya kama Musa alivyowaambia. Kwa hiyo wanaume 3,000 hivi waliuawa siku hiyo. **29** Kisha Musa akawaambia: “Jitakaseni* leo kwa ajili ya Yehova, kwa maana kila mmoja wenu amemshambulia mwana wake mwenyewe na ndugu yake mwenyewe;^e atawabariki leo.”^f

32:29 * Tnn., “Ujazeni mkono wenu.”

SURA YA 32

a Kut 15:24
Kut 16:2
Kut 17:2
Kum 9:7
Kum 31:27

b Kut 32:1
Mdo 7:40

c Yos 24:15
2Fa 10:15

d Hes 25:5

e Hes 25:11
Kum 13:6-9

f Kum 33:8, 9

Safu ya 2

a Hes 16:47
Hes 21:7
Kum 9:18

b Kut 20:23

c Hes 14:19

d Flp 4:3
Ufu 3:5

e Kut 23:20
Kut 33:2

SURA YA 33

f Mwa 12:7
Mwa 26:3

g Kut 23:20
Kut 32:34

h Kum 7:1, 22
Yos 24:11

i Kut 3:8
Kum 8:7-9

30 Siku iliyofuata, Musa akawaambia watu: “Mlitenda dhambi kubwa sana, na sasa nitapanda kwenda kwa Yehova ili nione ikiwa ninaweza kuomba msamaha kwa ajili ya dhambi yenu.”^a **31** Kwa hiyo Musa akarudi kwa Yehova na kumwambia: “Watu hawa wametenda dhambi kubwa sana! Walijitengeneza mungu wa dhahabu!”^b **32** Lakini sasa ukipenda, wasamehe dhambi yao;^c la sivyo, tafadhali nifute katika kitabu chako ulichoandika.”^d **33** Hata hivyo, Yehova akamwambia Musa: “Yeyote aliyenitendea dhambi, nitamfuta katika kitabu changu. **34** Nenda sasa, wangoze watu kwenda mahali nilipokuambia. Tazama! Malaika wangu atakutangulia,^e na siku ya kuwaadhibu itakapofika, nitawaadhibu kwa sababu ya dhambi yao.” **35** Ndipo Yehova akaanza kuwaletea watu pigo kwa sababu walikuwa wametengeneza sanamu ya ndama, sanamu ambayo Haruni alitengeneza.

33 Yehova akaendelea ku-mwambia Musa: “Ondoka mahali hapa pamoja na watu uliowaongoza kutoka katika nchi ya Misri. Safirini mpaka nchi niliyomwambia Abrahamu, Isaka, na Yakobo, niliposema, ‘Nitaupa uzao wenu* nchi hii.’^f **2** Nitamtu-ma malaika awatangulie^g na kuwafukuza Wakanaani, Waa-mori, Wahiti, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi.^h **3** Pandeni mpaka kwenye nchi inayotiririka maziwa na asali.ⁱ Lakini sitaenda pamoja nanyi, kwa sababu ninyi ni watu wakai-

33:1 * Tnn., “Nitaipa mbegu yenu.”

di,^a na huenda nikawaangamiza kabisa njiani.”^b

4 Watu waliposikia maneno hayo makali, wakaanza kuomboleza, na hakuna yeyote kati yao aliyevaa mapambo yake. **5** Yehova akamwambia Musa: “Waambie Waisraeli, ‘Ninyi ni watu wakaidi.’^c Ninaweza kupita mara moja katikati yenu na kuwaangamiza kabisa.”^d Sasa basi, msivae mapambo yenu ninapofikiria nitakavyowatendea.” **6** Kwa hiyo kuanzia Mlima Horebu na kuendelea, Waisraeli hawakuvaa* mapambo yao.

7 Sasa Musa akachukua hema lake na kulipiga nje ya kambi, mbali kidogo na kambi, naye akaliita hema la mkutano. Mtu yeyote aliyetafuta ushauri wa Yehova^e alikuwa akienda kwenye hema la mkutano, lililokuwa nje ya kambi. **8** Kila mara Musa alipokuwa akienda kwenye hema hilo, watu wote walitoka na kusimama kwenye mlango ya mahema yao, nao walimtaazama Musa mpaka alipoingia ndani ya hema hilo. **9** Kila mara Musa alipoingia katika hema hilo, ile nguzo ya wingu^f ilishuka chini na kusimama kwenye mlango wa hema hilo Mungu alipokuwa akiongea na Musa.^g **10** Watu wote walipoona nguzo hiyo ya wingu ikisimama kwenye mlango wa hema, kila mmoja wao alisimama na kuinama chini kwenye mlango wa hema lake. **11** Yehova aliongea na Musa uso kwa uso,^h kama mwanadamu anavyoongea na mwanadamu mwenzake. Musa alipo-

SURA YA 33

a Kut 32:9
Kum 9:6
Mdo 7:51

b Kut 32:10
Hes 16:21

c Kut 34:9
Kum 9:6
Mdo 7:51

d Hes 16:45

e Kut 18:25, 26
Hes 27:1-5

f Kut 13:21
Zb 99:7

g Hes 11:16, 17
Hes 12:5

h Kut 33:22, 23
Hes 12:8
Kum 34:10
Yoh 1:18
Yoh 6:46
Mdo 7:38

Safu ya 2

a Hes 11:28
Kum 1:38
Yos 1:1

b Kut 17:9
Kut 24:13

c Zb 25:4
Zb 27:11
Zb 86:11
Zb 119:33
Isa 30:21

d Kum 9:26

e Kut 13:21
Kut 40:34
Yos 1:5, 17
Isa 63:9

f Yos 21:44
Yos 23:1

g Hes 14:13, 14

h Kum 4:34
2Sa 7:23
Zb 147:20

i Kut 3:13
Kut 6:3
Kut 34:6

rudi kambini, Yoshua^a mwana wa Nuni, aliyekuwa mhudumu na mtumishi wake,^b haikuondoka hemani.

12 Sasa Musa akamwambia Yehova: “Angalia, unaniambia, ‘Waongoze watu hawa,’ lakini hujaniambia ni nani utakayemtuma pamoja nami. Isitoshe umeniambia, ‘Ninakujua kwa jina* na umepata kibali machoni pangu.’ **13** Tafadhali, ikiwa nimepata kibali machoni pako, nifundishe njia zako^c ili nikujue na kuendelea kuwa na kibali machoni pako. Pia, kumbuka kwamba taifa hili ni watu wako.”^d **14** Basi akasema: “Mimi mwenyewe nitakwenda* pamoja nawe,^e nami nitakupumzisha.”^f **15** Kisha Musa akamwambia: “Ikiwa wewe mwenyewe huendi* pamoja nasi, usituondoe mahali hapa. **16** Itajulikanaje kwamba mimi nimepata kibali machoni pako, mimi na watu wako? Je, haitajulikana ukionda pamoja nasi,^g ili mimi na watu wako tuonekane kuwa tofauti na watu wengine wote duniani?”^h

17 Yehova akaendelea kuwambia Musa: “Nitafanya pia jambo hilo unaloomba, kwa sababu umepata kibali machoni pangu nami nakujua wewe kwa jina.” **18** Ndi-po Musa akasema: “Tafadhali nionyeshe utukufu wako.” **19** Lakini akamwambia: “Nitafanya wema wangu wote upite mbele ya uso wako, nami nitatangaza jina langu Yehova mbele yako;ⁱ nami

33:3 *Au “wenye shingo ngumu.” 33:5 *Tnn., “wenye shingo ngumu.” 33:6 *Tnn., “waliyavua kabisa.”

33:12 *Au “Nimekuchagua.” 33:14 *Tnn., “Uso wangu utaenda.” 33:15 *Tnn., “Ikiwa uso wako hauendi.”

nitamwonyesha kibali yule ninayetaka kumwonyesha kibali, nami nitamwonyesha rehema yule ninayetaka kumwonyesha rehema.”^a **20** Lakini akasema: “Huwezi kuuona uso wangu, kwa sababu hakuna mwanadamu anayeweza kuniona na aendelee kuishi.”

21 Yehova akaendelea kusema: “Kuna mahali hapa karibu nami. Simama juu ya mwamba. **22** Utukufu wangu utakapokuwa ukipita, nitakuingiza kwenye shimo ndani ya mwamba, nami nitakuingiza kwa mkono wangu mpaka nitakapopita. **23** Kisha nitauondoa mkono wangu, nawe utauona mgongo wangu. Lakini uso wangu hautaonekana.”^b

34 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Jichongee mabamba mawili ya mawe kama yale ya kwanza,^c nami nitaandika kwenye mabamba hayo maneno yaliyokuwa kwenye yale mabamba ya kwanza^d uliyoyavunja.”^e **2** Jitayarishe kwa ajili ya asubuhi, kwa maana asubuhi utapanda Mlima Sinai na kusimama huko mbele zangu juu ya mlima huo.^f **3** Lakini mtu yeyote asipande pamoja nawe, na mtu mwingine yeyote asionekane popote mlimani. Hata mifugo haiipaswi kulisha mbele ya mlima huo.”^g

4 Basi Musa akachonga mabamba mawili ya mawe kama yale ya kwanza, akaamka asubuhi na mapema na kupanda Mlima Sinai, kama Yehova alivyomwamuru, akayabeba yale mabamba mawili ya mawe mikononi mwake. **5** Ndipo Yehova akashuka^h katika wingu na kusimama pamoja naye huko na kutangaza

SURA YA 33

a Ro 9:15

b Yoh 1:18

SURA YA 34

c Kum 10:1

d Kum 9:10

e Kut 32:19
Kum 9:17f Kut 19:20
Kut 24:12

g Kut 19:12, 13

h Mdo 7:38

Safu ya 2

a Kut 6:3
Kut 33:19

b Lu 6:36

c Kut 22:27
2Nya 30:9
Ne 9:17
Zb 86:15
Yoe 2:13d Hes 14:18
2Pe 3:9e Yer 31:3
Omb 3:22
Mlk 7:18f Zb 31:5
Ro 2:2

g Da 9:4

h Zb 103:12
Isa 55:7
Efe 4:32
1Yo 1:9i Kum 32:35
Yos 24:19
Ro 2:5
2Pe 2:4
Yud 14, 15j Kut 20:5
Kum 30:19
1Sa 15:2

k Kut 33:14

l Kut 32:9
Kut 33:3

m Hes 14:19

n 2Sa 7:23
Zb 147:19, 20o Kut 33:16
Kum 10:21p Kut 19:5, 6
Kum 12:28q Kut 3:8
Kut 33:2
Kum 7:1

jina lake, Yehova.^a **6** Yehova alipita mbele yake akitangaza: “Mimi Yehova, Yehova, ni Mungu mwenye rehema^b na huruma,^c si mwepesi wa hasira,^d nina upendo mwingi mshikamanifu^e na kweli,^f **7** ninawatendea maelfu kwa upendo mshikamanifu,^g ninasamehe makosa na uovu na dhambi,^h lakini sikosi kamwe kuwaadhibu wenye hatia,ⁱ ninawaadhibu wana na wajukuu kufikia kizazi cha tatu na cha nne kwa sababu ya makosa ya baba zao.”^j

8 Musa akainama haraka mpaka chini na kusujudu. **9** Kisha akasema: “Ikiwa sasa nimepata kibali machoni pako, Ee Yehova, sasa tafadhali, Yehova, nenda pamoja nasi uwe kati yetu,^k ingawa sisi ni watu wakaidi,^l utusamehe makosa yetu na dhambi zetu,^m nawe utuchukue kuwa mali yako mwenyewe.” **10** Naye akasema: “Tazama, ninafanya agano: Nitafanya mbele ya watu wako wote mambo yanayostaajibisha ambayo sijawahi kamwe kuyafanya* katika dunia yote wala kati ya mataifa yote,ⁿ na watu wote mnaoishi miongoni mwao wataona kazi yangu mimi, Yehova, kwa sababu nitafanya jambo linaloogopesha kwa ajili yenu.”^o

11 “Sikilizeni mambo ninayowaamuru leo.^p Tazama, ninawafukuza Waamori, Wakanani, Wahiti, Waperizi, Wahiwi, na Wayebusi^q kutoka mbele yenu. **12** Muwe waangalifu msifanye agano na wakaaji wa

34:6 *Au “neema.” #Au “fadhili zenye upendo.” ^aAu “uaminifu.” **34:9** *Au “wenye shingo ngumu.” **34:10** *Au “kuyaumba.”

nchi mnayoenda kuingia,^a ili agano hilo lisiwe mtego kweni.^b **13** Lakini mtabomoa madhabahu zao, mtazivunjanvuna nguzo yao takatifu, na kuitaka mizi yao mitakatifu.*^c

14 Msimwinamie mungu mwingine,^d kwa sababu mimi Yehova ninajulikana kuwa Mungu ninayetaka* watu waniabudu mimi peke yangu.[#] Naam, mimi ni Mungu ninayetaka watu waniabudu mimi peke yangu.^e **15** Muwe waangalifu msifanye agano na wakaaji wa nchi, kwa maana wanapofanya ukahaba na miungu yao na kuitolea dhabihu,^f mmoja wao atawaalika nanyi mtakula dhabihu yake.^g **16** Kisha kwa hakika mtawachukua baadhi ya mabinti wao ili waoleme na wana wenu,^h na mabinti wao watafanya ukahaba na miungu yao na kusababisha wana wenu wafanye ukahaba na miungu yao.ⁱ

17 "Hampaswi kutengeneza miungu ya chuma.^j

18 "Mnapaswa kuadhimisha Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu.^k Mtakula mikate isiyo na chachu, kama nilivyowaamuru; mtaila kwa siku saba wakati uliowekwa katika mwezi wa Abibu,*^l kwa sababu mlitoka Misri katika mwezi wa Abibu.

19 "Kila mzaliwa wa kwanza wa kiume* ni wangu,^m kutia ndani mifugo yenu yote, iwe ni ng'ombe dume wa kwanza au kondoo.ⁿ **20** Mtamkomboa mzaliwa wa kwanza wa punda kwa kondoo. Laki-

34:13 *Angalia Kamusi, uku. 2012. **34:14** *Tnn., "Yehova, jina langu lina-dai." [#]Au "nisiyevumilia washindani." **34:18** *Angalia Nyongeza B15. **34:19** *Tnn., "Kila kifungua mimba."

SURA YA 34

a Kum 7:2

b Kut 23:32, 33

c Kut 23:24
Kum 12:3d Kut 20:3
1Ko 10:14
1Yo 5:21

e Yos 24:19

f 1Ko 10:20

g Hes 25:2
2Ko 6:14

h Ezr 9:2

i Kum 7:4
Kum 31:16
Amu 2:17
Amu 8:33
1Fa 11:2
Ne 13:26
Zb 106:28j Kut 32:8
Law 19:4

k Law 23:6

l Kut 23:15

m Kut 13:2
Lu 2:23

n Kut 22:30

Safu ya 2

a Kut 13:15
Hes 18:15, 16

b Kum 5:12

c Kut 23:16
Law 23:34

d Kum 16:16

e Kut 34:11

f Kut 23:18

g Kut 12:10
Hes 9:12h Hes 18:8, 12
Kum 26:2
Met 3:9i Kut 23:19
Kum 14:21

ni msipomkomboa, basi mtamvunja shingo. Mnapaswa kumkomboa kila mzaliwa wenu wa kwanza kati ya wana wenu.^a Mtu yeyote asiye mbele zangu mikonu mitupu.

21 "Kwa siku sita mtafanya kazi, lakini siku ya saba mtapumzika.*^b Mtapumzika hata wakati wa kulima na wa kuvuna.

22 "Nanyi mtafanya Sherehe yenu ya Majuma kwa kutumia mavuno ya kwanza ya ngano iliyokomaa, na pia Sherehe ya Kukusanya* mwishoni mwa mwaka.^c

23 "Mara tatu kwa mwaka, wanaume wenu wote wanapaswa kwenda mbele za Bwana wa kweli, Yehova, Mungu wa Israeli.^d **24** Kwa maana nitayafukuza mataifa kutoka mbele yenu,^e nami nitapanua eneo lenu, na hakuna mtu atakayetamani nchi yenu mtakapokuwa mkipanda kwenda mbele za* Yehova Mungu wenu mara tatu kwa mwaka.

25 "Hampaswi kutoa damu ya dhabihu yangu pamoja na kitu chochote kilichotiwa chachu.^f Dhabihu ya sherehe ya Pasaka haipaswi kuhifadhiwa usiku kucha mpaka asubuhi.^g

26 "Mazao bora ya kwanza yaliyokomaa* ya ardhi yenu mnapaswa kuyaleta katika nyumba ya Yehova Mungu wenu.^h

"Msimchemshe mwanambuzi katika maziwa ya mama yake."ⁱ

34:21 *Au "mtashika sabato." **34:22** *Pia inaitwa Sherehe ya Vibanda (Mahema). **34:24** *Tnn., "kuuona uso wa." **34:26** *Au "Matunda ya kwanza bora yaliyoiva."

27 Yehova akaendelea ku-mwambia Musa: “Unapaswa kuandika maneno haya,^a kwa sababu kulingana na maneno haya, ninafanya agano pamoja nawe na pamoja na Israeli.”^b 28 Musa akaendelea ku-kaa huko pamoja na Yehova kwa siku 40, mchana na usiku. Hakula mkate wala kunywa maji.^c Naye Mungu aliandika kwenye yale mabamba, maneno ya agano hilo, zile Amri Kumi.*^d

29 Basi Musa akashuka Mlima Sinai akiwa amebeba mikononi yale mabamba mawili^e ya Ushahidi. Aliposhuka mlimani, Musa hakujua kwamba ngozi ya uso wake ilikuwa iki-toa miale kwa sababu alikuwa ameongea na Mungu. 30 Haruni na Waisraeli wote walipomtazama Musa, waliona kwamba ngozi ya uso wake ilikuwa ikitoa miale, wakaogopa kumkaribia.^f

31 Lakini Musa akawaita, kwa hiyo Haruni na wakuu wote wa kusanyiko wakamkaribia, naye Musa akaongea nao. 32 Baada ya hayo Waisraeli wote wakamkaribia, naye akawapa amri zote alizopewa na Yehova kwenye Mlima Sinai.^g 33 Musa alipomaliza kuongea nao, alikuwa akiufunika uso wake kwa kitambaa.^h 34 Lakini kila mara Musa alipoingia ndani mbele za Yehova ili kuongea naye, alikivua kitambaa hicho lakini alijifunika alipotoka nje.ⁱ Alipotoka nje aliwajulisha Waisraeli amri zote alizopewa.^j 35 Nao Waisraeli waliona kwamba ngozi ya uso wa Musa ilitoa miale; basi Musa alijifu-

34:28 *Tnn., “yale Maneno Kumi.”

SURA YA 34

a Kut 24:4

Kum 31:9, 11

b Kut 24:8

Kum 4:13

c Kum 9:18

d Kut 31:18

Kum 10:2

e Kut 32:15

f 2Ko 3:7

g Kut 24:3

Kum 1:3

h 2Ko 3:13

i 2Ko 3:16

j Kum 27:10

Safu ya 2

a 2Ko 3:7, 13

SURA YA 35

b Kut 34:32

c Kut 20:9, 10

Law 23:3

d Kut 31:14, 15

Hes 15:32, 35

e Kut 25:2-7

Kut 35:29

f 2Ko 8:12

2Ko 9:7

g Kut 26:7

Kut 36:8

h Kut 25:3, 6

i Kut 28:9

Kut 39:14

j Kut 28:15

k Kut 31:6

Kut 36:1

nika tena kitambaa hicho usoni alipotoka na kukivua alipoingia kuzungumza na Mungu.^a

35 Baadaye Musa akaliku-sanya pamoja kusan-nyiko lote la Waisraeli na ku-liambia: “Haya ndiyo mambo ambayo Yehova ameamuru ya-fanywe.”^b 2 Mtafanya kazi kwa siku sita, lakini siku ya saba itakuwa takatifu kwe-nu, ni sabato ya pumziko ka-mili kwa Yehova.^c Mtu yeyo-te atakayefanya kazi siku hiyo atauawa.^d 3 Hampaswi kuwasha moto katika makao yenu yoyote siku ya Sabato.”

4 Kisha Musa akaliambia kusanyiko lote la Waisraeli: “Yehova ameamuru hivi: 5 ‘Mtoleeni Yehova mchango kutoka miongoni mwe-nu.^e Kila mtu aliye na moyo wa kutoa kwa hiari^f na amle-tee Yehova mchango wa dha-habu, fedha, shaba, 6 nyuzi za bluu, sufu ya zamba-rau, kitambaa cha rangi nye-kundu, kitani bora, manyo-ya ya mbuzi,^g 7 ngozi za ko-ndoo dume zilizotiwa rangi nyekundu, ngozi za sili, mbao za mshita, 8 mafuta kwa aji-li ya taa, mafuta ya zeri ya ku-tengenezea mafuta yanayotu-miwa kutia mafuta na uvumba uliotiwa manukato,^h 9 mawe ya shohamu, na mawe mengi-ne ya kupambia efodiⁱ na kifuko cha kifuani.^j

10 “Watu wote ambao ni stadi*^k kati yenu na waje kutengeneza kila kitu ambacho Yehova ameamuru, 11 yaani, hema la ibada na kifuniko chake, kulabu zake na viu-nzi vyake vya mbao, fito zake, nguzo zake, na vikalio

35:10 *Au “wenye hekima moyoni.”

vyake; **12** Sanduku la Agano^a na fito zake,^b kifuniko,^c na pazia^d linalofunika sanduku hilo; **13** meza^e na fito zake na vyombo vyake vyote na mikate ya wonyesho;^f **14** kinara cha taa^g na vyombo vyake na taa zake na mafuta yake;^h **15** madhabahu ya uvumbaⁱ na fito zake; mafuta yanayotumiwa kutia mafuta na uvumba uliotiwa manukato;^j pazia la mlango wa hema la ibada; **16** madhabahu ya dhahabu za kuteketezwa^k na wavu wake wa shaba, fito zake na vyombo vyake vyote; beseni na kinara chake;^l **17** mapazia ya ua yanayoning'inia,^m nguzo zake na vikalio vyake; pazia la mlango wa ua; **18** vingi vya hema la ibada na vingi vya ua na kamba zake;ⁿ **19** mavazi yaliyofumwa kwa ustadi^o ya kuhudumu mahali patakatifu, mavazi matakatifu ya kuhani Haruni,^p na mavazi ya wanawe ya kutumikia wakiwa makuhani.”

20 Kwa hiyo kusanyiko lote la Waisraeli likaondoka mbele ya Musa. **21** Basi kila mtu ambaye moyo wake ulimsukuma^q na kila mtu aliyechochewa na roho yake akaja na kumletea Yehova mchango ili utumiwe katika kazi ya hema la mkutano, yaani, katika utumishi wake wote, na kwa ajili ya mavazi matakatifu. **22** Nao wakaendelea kuja, wanaume pamoja na wanawake, kila mtu aliyekuwa na moyo wa kutoa kwa hiari akaleta bizimu, vipuli, pete, na vito vingine, kutia ndani vito vya dhahabu vya kila aina. Wote wakamletea Yehova matoleo yao* ya dhahabu.

35:22 *Au “matoleo yao ya kutikiswa.”

SURA YA 35

a Kut 25:10

b Kut 25:13

c Kut 25:17

d Kut 26:31

e Kut 25:23

f Kut 25:30
Law 24:5, 6

g Kut 25:31

h Kut 27:20

i Kut 30:1
Kut 37:25
Kut 40:5

j Kut 30:34, 35

k Kut 27:1

l Kut 30:18
Kut 38:8

m Kut 27:9

n Kut 27:19

o Kut 31:6, 10
Kut 39:33, 41

p Kut 39:1

q Kut 25:2
Kut 36:2
2Ko 8:12
2Ko 9:7

r Kut 38:24

r Kut 38:24

Safu ya 2

a Kut 28:3

Kut 31:6
Kut 36:8b Kut 28:15, 28
Kut 39:15, 21

c Kut 30:23-25

d Kut 30:34, 35

e Kut 36:5
2Ko 9:7

f Kut 31:2-6

23 Na wote waliokuwa na nyuzi za bluu, sufu ya zambaurau, kitambaa cha rangi nyekundu, kitani bora, manyoya ya mbuzi, ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu, na ngozi za sili, wakaleta vitu hivyo. **24** Wote walioitoa fedha na shaba wakaleta mchango wa Yehova, na wote waliokuwa na mbao za mshita za kutumiwa katika kazi yoyote ile wakazileta.

25 Wanawake wote wenye ustadi^a wa kusokota wakasokota kwa mikono yao na kuleta vitu walivyosokota: nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora. **26** Na wanawake wote wenye ustadi ambao walisukumwa na mioyo yao wakasokota manyoya ya mbuzi.

27 Nao wakuu wakaleta mawe ya shohamu na mawe mengine ya kupambia efodi na kifuko cha kifuni,^b **28** na mafuta ya zeri na mafuta kwa ajili ya taa na ya kutumiwa kutengeneza mafuta ya kutia mafuta^c na kwa ajili ya uvumba uliotiwa manukato.^d **29** Wanaume na wanawake wote waliochochewa na mioyo yao wakaleta kitu fulani kwa ajili ya kazi ambayo Yehova alimwamuru Musa ifanywe; Waisraeli walimletea Yehova vitu hivyo vikiwa toleo la hiari.^e

30 Kisha Musa akawaambia Waisraeli: “Tazameni, Yehova amemchagua Bezaleli mwana wa Uri mwana wa Huru wa kabila la Yuda.^f **31** Amemjaza roho ya Mungu, amemjaza hekima, ulewaji, na ujuzi katika kila aina ya ufundi **32** ili abuni kazi za

usanii akitumia dhahabu, fedha, na shaba, **33** ili achange na kupamba kwa mawe, na kutengeneza vifaa vya mbao vya kila aina kwa usanii. **34** Naye ameweka moyoni mwake ustadi wa kufundisha, yeye na Oholiabu^a mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani. **35** Amewajaza ustadi wa^{*b} kufanya kazi zote za ufundi, kutarizi, na kufuma kwa nyuzi za bluu, safu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora, na kazi zote za mfumaji. Wanau-me hao watafanya kazi za kila aina na kubuni vyombo vya kila aina kwa ufundi.

36 “Bezaleli atafanya kazi pamoja na Oholiabu na kila mtu mwenye ustadi* ambaye Yehova amempa hekima na uelewaji ili kujua jinsi ya kufanya utumishi wote mtakatifu kama Yehova alivyoamuru.”^c

2 Kisha Musa akamwita Bezaleli na Oholiabu na kila mtu mwenye ustadi ambaye Yehova aliweka hekima moyoni mwake,^d kila mtu ambaye moyo wake ulimsukuma kujitolea kufanya kazi.^e **3** Basi wakachukua kutoka kwa Musa mchango wote^f ambao Waisraeli walileta kwa ajili ya utumishi mtakatifu. Hata hivyo, watu wakaendelea kumletea matoleo ya hiari, asubuhi baada ya asubuhi.

4 Walipoanza kufanya kazi takatifu, mafundi wote wenyewe ustadi wakaja, mmoja baada ya mwingine, **5** nao walikuwa wakimwambia Musa: “Watu wanaleta vitu vingi sana kuliko vinavyohitaji-

35:35 *Au “hekima moyoni ya.” 36:1 *Au “mwenye hekima moyoni.”

SURA YA 35

a Kut 36:1

b Kut 31:3

SURA YA 36

c Kut 25:9
Kut 31:6

d Kut 28:3
Kut 35:10

e Kut 35:21, 26

f Kut 35:5-9
Met 3:9
Zko 9:7

Safu ya 2

a Kut 31:6

b Kut 25:9
Kut 39:32
Ebr 9:9

c Kut 26:1-6

ka kwa ajili ya kazi ambayo Yehova ameamuru ifanywe.” **6** Kwa hiyo Musa akaamuru kwamba tangazo litolewe kote kote kambini, likisema: “Wanau-me na wanawake, msilete vitu zaidi kwa ajili ya mchango mtakatifu.” Basi watu wakazuiwa wasilete tena kitu chochote. **7** Vitu walivyoleta vilitosha kukamilisha kazi yote iliyopaswa kufanywa, tena vilizidi.

8 Kwa hiyo mafundi wote stadi^a walitengeneza hema la ibada^b kwa vitambaa kumi vya kitani bora kilichosokotwa, kwa nyuzi za bluu, safu ya zambarau, na kitambaa cha rangi nyekundu; akavitarizi* kwa michoro ya makerubi.^c

9 Kila kitambaa cha hema la ibada kilikuwa na urefu wa mikono 28* na upana wa mikono 4. Vitambaa vyote vilikuwa na ukubwa uleule.

10 Akaviunganisha pamoja vitambaa vitano vya hema, na pia akaviunganisha pamoja vile vitambaa vingine vitano. **11** Kisha akatengeneza vitanzi vya nyuzi za bluu kwenye upindo wa kitambaa cha mwisho. Naye akafanya vivyo hivyo kwenye upindo wa kitambaa kile kingine cha mwisho mahali ambapo vingeanishwa. **12** Akatengeneza vitanzi 50 kwenye kitambaa kimoja na vitanzi vingine 50 kwenye upindo wa kitambaa cha pili ili vitanzi hivyo vielekeane vinapounganishwa. **13** Hatimaye, akatengeneza vibanio 50 vya dhahabu na kviunganisha vita-

36:8 *Inaonekana ni Bezaleli. 36:9 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

mbaa hivyo pamoja kwa vibanio hivyo, basi hema la ibada likawa na kitambaa kimoja kizima.

14 Kisha akatengeneza vitambaa vya manyoya ya mbuzi vya kufunika hema hilo. Akatengeneza vitambaa 11 vya hema.^a **15** Kila kitambaa kilikuwa na urefu wa mikono 30 na upana wa mikono 4. Vitambaa vyote 11 vilikuwa na ukubwa uleule. **16** Kisha akaunganisha vitambaa vitano pamoja na vile vitambaa vingine sita pamoja. **17** Hala-fu akatengeneza vitanzi 50 kwenye upindo wa kitambaa cha kwanza, kwenye kipande cha mwisho kabisa, na vitanzi 50 kwenye upindo wa kitambaa cha pili, mahali vinapounganishwa. **18** Naye akatengeneza vibanio 50 vya shaba vya kuunganisha hema pamoja ili liwe na kitambaa kimoja kizima.

19 Akatengeneza kifuniko cha hema kwa kutumia ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu na juu yake kifuniko cha ngozi za sili.^b

20 Kisha akatengeneza viunzi vya mbao za mshita^c vilivyo wima kwa ajili ya hema hilo.^d **21** Kila kiunzi kilikuwa na urefu wa mikono kumi na upana wa mkono mmoja na nusu. **22** Kila kiunzi kilikuwa na ndimi mbili* zilizounganishwa pamoja. Hivyo ndivyo alivyotengeneza viunzi vyote vya hema la ibada. **23** Kwa hiyo alitengeneza viunzi 20 kwa ajili ya upande wa kusini wa hema la ibada. **24** Kisha akatengeneza vikaliyo 40 vya fedha chini ya vile viunzi 20: vikaliyo viwili chini ya

SURA YA 36

a Kut 26:7-11

b Kut 26:14

c Kut 25:10, 23
Kut 27:1
Kut 30:5
Kut 36:36

d Kut 26:15-18

Safu ya 2

a Kut 26:19-21

b Kut 26:22-25

c Kut 26:26-28

d Kut 26:29

e Kut 40:21
Ebr 10:19, 20

kiunzi kimoja pamoja na ndimi zake mbili na vikaliyo vingine viwili chini ya kila kiunzi kilichofuata pamoja na ndimi zake mbili.^a **25** Akatengeneza viunzi 20 upande wa pili wa hema, upande wa kaskazini **26** pamoja na vikaliyo vya-ke 40 vya fedha, vikaliyo viwili chini ya kiunzi kimoja na vikaliyo viwili chini ya kila kiunzi kilichofuata.

27 Akatengeneza viunzi sita sehemu ya nyuma ya hema la ibada, upande wa magharibi.^b **28** Naye akatengeneza viunzi viwili viwe mihimili miwili ya pembeni upande wa nyuma wa hema la ibada. **29** Katika pembe zote mbili kulikuwa na viunzi viwili kuanzia sehemu ya chini mpaka sehemu ya juu, kwenye pete ya kwanza. Hivyo ndivyo alivyotengeneza ile mihimili miwili ya pembeni. **30** Kwa ujumla kulikuwa na viunzi vinane na vikaliyo vyake 16 vya fedha, vikaliyo viwili chini ya kila kiunzi.

31 Kisha akatengeneza fito za mshita, fito tano kwa ajili ya viunzi vya upande mmoja wa hema la ibada^c **32** na fito tano kwa ajili ya viunzi vya upande wa pili wa hema la ibada na fito tano kwa ajili ya viunzi vya sehemu ya nyuma ya hema la ibada, upande wa magharibi. **33** Akatengeneza ufito katikati ya viunzi kutoka mwisho mmoja mpaka mwisho mwingine. **34** Akavifunika viunzi hivyo kwa dhahabu, akatengeneza pete za dhahabu ili zishikilie zile fito, naye akazifunika fito hizo kwa dhahabu.^d

35 Kisha akatengeneza pazia^e la nyuzi za bluu, sufu

ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa. Akalitarizi^a kwa michoro ya makerubi.^b **36** Kisha akalitengeneza nguzo nne za mshita na kuzifunika kwa dhahabu, akatengeneza pia kulabu za dhahabu na vikaliyo vinne vya fedha kwa ajili ya nguzo hizo. **37** Halafu akatengeneza pazia la mlango wa hema kwa nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa na kufumwa.^c **38** na pia nguzo zake tano na vibanio vyake. Akafunika kwa dhahabu sehemu ya juu ya nguzo hizo pamoja na kulabu* zake, lakini vikaliyo vyake vitano vilikuwa vya shaba.

37 Kisha Bezaleli^d akatengeneza sanduku la agano^e kwa mbao za mshita. Lili kuwa na urefu wa mikono miwili na nusu* na upana wa mkono mmoja na nusu na kimo cha mkono mmoja na nusu.^f **2** Akalifunika ndani na nje kwa dhahabu safi na kutengeneza ukingo wa dhahabu kulizunguka.^g **3** Kisha akalitengeneza pete nne za dhahabu na kuzifunga sehemu ya juu ya miguu yake minne, pete mbili upande mmoja na pete mbili upande wa pili. **4** Halafu akatengeneza fito za mshita na kuzifunika kwa dhahabu.^h **5** Akazitia fito hizo kwenye zile pete zilizo pande mbili za Sanduku hilo ili zitumiwe kulibeba.ⁱ

6 Akatengeneza kifuniko cha dhahabu safi.^j Kilikuwa

36:38 *Au "pete; vitanzi; vibanio" vya kushikia. **37:1** *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 36

a Kut 26:31, 32

b Mwa 3:24

c Kut 26:36, 37

SURA YA 37

d Kut 31:2-5
Kut 38:22e Kut 40:3
Hes 10:33

f Kut 25:10-15

g Ebr 9:4

h 2Nya 5:9

i Yos 3:8

j Law 16:2, 14
1Nya 28:11

Safu ya 2

a Kut 25:17-20

b Mwa 3:24

c Kut 40:20

d Ebr 9:5

e 1Sa 4:4
Zb 80:1

f Kut 40:4

g Kut 25:23-28

h Kut 25:29

na urefu wa mikono miwili na nusu na upana wa mkono mmoja na nusu.^a **7** Kisha akatengeneza makerubi wawili^b wa dhahabu kwa nyundo kwenye miisho miwili ya kifuniko hicho.^c **8** Kerubi mmoja alikuwa kwenye mwisho mmoja, na yule kerubi mwingine kwenye mwisho wa pili wa kifuniko. Alitengeneza makerubi hao kwenye pande zote mbili za kifuniko. **9** Makerubi hao walikuwa wamenyoo-sha mabawa yao kuelekea juu, na hivyo kukifunika kifuniko hicho kwa mabawa yao.^d Walielekeana huku nyuso zao zikitazama kifuniko.^e

10 Kisha akatengeneza meza ya mbao za mshita.^f Ilikuwa na urefu wa mikono miwili, upana wa mkono mmoja, na kimo cha mkono mmoja na nusu.^g **11** Akaifunika kwa dhahabu safi na kutengeneza ukingo wa dhahabu kuizunguka. **12** Kisha akatengeneza utepe wenye upana wa kiganja kimoja* kuizunguka na ukingo wa dhahabu kuzunguka utepe huo. **13** Pia, akatengeneza pete nne za dhahabu na kuzitia kwenye pembe nne za miguu yake minne. **14** Pete hizo zilikuwa karibu na utepe ili fito za kubeba meza hiyo zitiwe humo. **15** Halafu akatengeneza fito za mshita na kuzifunika kwa dhahabu ili zitumiwe kubeba meza hiyo. **16** Baada ya hayo akatengeneza sahani, vikombe, magudulia, na mabakuli ya meza hiyo kwa dhahabu safi ili yatumiwe kumimina matoleo ya vinywaji.^h

37:12 *Karibu sentimita 7.4 (inchi 2.9). Angalia Nyongeza B14.

17 Halafu akatengeneza kinara cha taa kwa dhahabu safi.^a Alikitengeneza kinara hicho cha taa kwa nyundo. Sehemu yake ya chini, shina lake, matawi yake, vikombe vyake, matumba yake, na maua yake yalitengenezwa kwa kipande kimoja cha dhahabu.^b 18 Kinara hicho kilikuwa na matawi sita, matawi matatu upande mmoja na matawi matatu upande wa pili. 19 Kila tawi lilikuwa na vikombe vitatu vyenye umbo la maua ya mlozi, na kila kikombe kilikuwa na ua na tumba lake. Hivyo ndivyo matawi hayo sita yalivyotengenezwa kwenye shina la kinara hicho cha taa. 20 Shina la kinara lilikuwa na vikombe vine vyenye umbo la maua ya mlozi, kila kikombe kilikuwa na ua na tumba lake. 21 Kuli kuwa na tumba chini ya jozi ya kwanza ya matawi hayo sita, tumba chini ya jozi ya pili, na tumba chini ya jozi ya tatu. 22 Matumba na matawi yake na kinara chote cha taa kilite ngenezwa kwa kipande kimoja cha dhahabu safi, kwa kutumia nyundo. 23 Kisha akatengeneza taa saba^c pamoja na koleo zake na vyetezo vyake kwa dhahabu safi. 24 Alitumia talanta moja* ya dhahabu safi kutengeneza kinara hicho na vifaa vyake vyote.

25 Kisha akatumia mbao za mshita kujenga madhabahu ya kufukizia uvumba.^d Ilikuwa ya mraba, yenye urefu wa mkono mmoja, upana wa mkono mmoja, na kimo cha mikono miwili. Pembe zake zilikuwa sehemu ya hiyo madhaba-

37:24 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 37

a Kut 40:24
Law 24:4
2Nya 13:11

b Kut 25:31-39

c Hes 8:2

d Kut 30:7
Kut 40:5
Zb 141:2
Ufu 8:3

Safu ya 2

a Kut 30:1-5

b Kut 30:25, 33
Kut 40:9

c Kut 30:34, 35
Zb 141:2

SURA YA 38

d Kut 27:1-8
Kut 40:10

hu.^a 26 Aliifunika kwa dhahabu safi sehemu yake ya juu, pande zote kuizunguka na pia pembe zake, na kutengeneza ukingo wa dhahabu kuizunguka. 27 Akaitengeneza pete mbili za dhahabu chini ya ukingo wake kwenye pande zake mbili zinazoelekeana ili zishikilie fito za kubebea madhabahu. 28 Baada ya hayo akatengeneza fito za mshita na kuzifunika kwa dhahabu. 29 Alitengeneza pia mafuta matakafu ya kutia mafuta^b na uvumba safi uliotiwa manukato^c na kuchanganywa kwa ustadi.*

38 Akatumia mbao za mshita kutengeneza madhabahu ya dhahabu za kuteketezwa. Ilikuwa ya mraba, yenye urefu wa mikono mitano,^{*} upana wa mikono mitano, na kimo cha mikono mitatu.^d

2 Kisha akatengeneza pembe kwenye ncha zake nne. Pembe hizo zilikuwa sehemu ya hiyo madhabahu. Naye akaifunika kwa shaba.^e 3 Baada ya hayo akatengeneza vyombo vyote vya madhabahu: ndoo za kuondolea majivu, sepetu, mabakuli, nyuma,^{*} na vyetezo. Alitengeneza vyombo hivyo vyote kwa shaba. 4 Pia, alitengeneza wavu wa shaba kwa ajili ya madhabahu, chini ya ukingo wake, katikati ya madhabahu. 5 Alitengeneza pete nne kwenye pembe nne za wavu huo karibu na wavu huo wa shaba, ili zishikilie fito. 6 Baada ya hayo akatengeneza fito kwa mbao za

37:29 *Au "kama anavyofanya mtengenezaji wa manukato." 38:1 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. 38:3 *Wingi wa kifaa kinachoitwa uma.

e 2Nya 1:5

mshita na kuzifunika kwa shaba. **7** Kisha akazitia fito hizo kwenye zile pete zilizo kwenye pande za madhabahu ili zitumiwe kubebea madhabahu. Alitengeneza madhabahu hiyo kama sanduku la mbao lenye uwazi.

8 Kisha akatengeneza beseni la shaba^a na kinara chake cha shaba; alitumia vioo* vya wanawake waliotumikia kwenye mlango wa hema la mkutano kulingana na mpangilio uliowekwa.

9 Kisha akatengeneza ua.^b Upande wa kusini wa ua huo, alitengeneza mapazia yanayoning'inia ya kitani bora kilichosokotwa yenye urefu wa mikono 100.^c **10** Ulikuwa na nguzo 20 na vikaliyo 20 vya shaba, na kulabu za nguzo hizo na vitanzi* vyake vilikuwa vya fedha. **11** Pia, kulikuwa na mapazia yanayoning'inia upande wa kaskazini yenye urefu wa mikono 100. Nguzo zake 20 na vikaliyo vya-ke 20 vilikuwa vya shaba. Lakini kulabu za nguzo hizo na vitanzi* vyake vilikuwa vya fedha. **12** Hata hivyo, upande wa magharibi ulikuwa na mapazia yanayoning'inia yenye urefu wa mikono 50. Pia ulikuwa na nguzo kumi na vikaliyo kumi, kulabu na vitanzi* vyake vilikuwa vya fedha. **13** Ua huo ulikuwa na upana wa mikono 50 upande wa mashariki, yaani, upande wa mapambazuko ya jua. **14** Upande mmoja ulikuwa na mapazia yanayoning'inia yenye upana wa mikono 15, pamoja na nguzo tatu na vikaliyo vitatu.

38:8 *Yaani, vioo vya shaba vilivyoning'arishwa sana. **38:10-12, 17, 19** *Au "pete; vitanzi; vibanio" vya kushikia.

SURA YA 38

a Kut 30:18
Law 8:11
1Fa 7:23

b Kut 40:8

c Kut 27:9-15

Safu ya 2

a Kut 27:17

b Kut 27:16

c Kut 27:19

d Kut 25:16
Kut 31:18
Hes 17:7

e Hes 3:6
Hes 4:46, 47

f Kut 6:23
Hes 4:28
1Nya 6:3

g Kut 31:2-5
Kut 35:30
Kut 36:1
Kut 37:1
2Nya 1:5

h Kut 31:6
Kut 35:34
Kut 36:2

15 Upande wa pili wa mlango wa ua ulikuwa na mapazia yanayoning'inia yenye upana wa mikono 15, pamoja na nguzo tatu na vikaliyo vyake vitatu. **16** Mapazia yote yanayoning'inia kuzunguka ua yalitengenezwa kwa kitani bora kilichosokotwa. **17** Vikaliyo vya nguzo vilikuwa vya shaba, kulabu za nguzo hizo na vitanzi* vyake vilikuwa vya fedha, sehemu za juu zilifunika kwa fedha, na nguzo zote za ua zilikuwa na kulabu za fedha.^a

18 Pazia la mlango wa ua lilifumwa kwa nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa. Likuwa na urefu wa mikono 20 na kimo cha mikono 5, sawa na kimo cha mapazia ya ua yanayoning'inia.^b **19** Nguzo zake nne na vikaliyo vyake vinnе vilikuwa vya shaba. Kulabu zake na vitanzi* vyake vilikuwa vya fedha, na sehemu zake za juu zilifunikwa kwa fedha. **20** Vigingi vyote vya hema la ibada na vya ua vilikuwa vya shaba.^c

21 Ifuatayo ni orodha ya vitu vilivyotumiwa kutengeneza hema la ibada, yaani, hema la Ushahidi.^d Orodha hii ilitayarishwa kwa amri ya Musa, na lilikuwa jukumu la Walawi^e kuitayarisha chini ya uongozi wa Ithamari^f mwana wa Haruni kuhani. **22** Bezaleli^g mwana wa Uri mwana wa Huru wa kabila la Yuda alifanya mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Musa. **23** Alikuwa pamoja na Oholiab^h mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani, aliyekuwa fundi, mtarizi, na

mfumaji wa nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora.

24 Dhahabu yote iliyotumiwa kwa kazi zote za mahali patakatifu ndiyo dhahabu yote iliyotolewa kama toleo la kutikiswa,^a ilikuwa talanta 29* na shekeli 730[#] kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.^Δ **25** Fedha iliyotolewa na wale walioandikishwa ilikuwa talanta 100 na shekeli 1,775 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.^Δ **26** Nusu shekeli iliyotolewa na kila mwanamume ilikuwa nusu shekeli kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^Δ litolewa na kila mwanamume aliyeandikishwa mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi,^b wote walikuwa 603,550.^c

27 Talanta 100 za fedha zilitumiwa kutengeneza vikaliyo vya mahali patakatifu na vikaliyo vya pazia; talanta 100 zilitumiwa kutengeneza vikaliyo 100, talanta moja kwa kila kikalio.^d **28** Alitumia zile shekeli 1,775 kutengeneza kulabu za nguzo na kufunika sehemu zake za juu na kuziunganisha pamoja.

29 Shaba iliyotolewa ikiwa toleo* ilikuwa talanta 70 na shekeli 2,400. **30** Alitumia shaba hiyo kutengeneza vikaliyo vya mlango wa hema la mkutano, madhabahu ya shaba na wavu wake wa shaba, vyombo vyote vya madha-

38:24 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. [#]Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. **38:24-26** ^ΔAu "shekeli patakatifu." **38:29** *Au "toleo la kutikiswa."

SURA YA 38

a Kut 35:22

b Kut 30:15

c Kut 12:37
Hes 1:45, 46

d Kut 26:19-21
Kut 26:25, 32

Safu ya 2

a Kut 27:19

SURA YA 39

b Kut 35:23

c Kut 28:4, 5
Kut 29:5
Kut 35:10, 19

d Kut 28:6-8
Law 8:7

e Kut 29:5

f Kut 28:9, 10

bahu, **31** vikaliyo vyote vya ua, vikaliyo vya mlango wa ua, vingingi vyote vya hema la ibada, na vingingi vyote^a vya ua.

39 Walitumia zile nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, na kitambaa cha rangi nyekundu^b kufuma kwa ustadi mavazi ya kuhudumu mahali patakatifu. Walimtengeneza Haruni mavazi matakatifu^c kama Yehova alivyomwamuru Musa.

2 Alitengeneza* efodi^d kwa dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa. **3** Walitengeneza mabamba mabamba ya dhahabu kwa kutumia nyundo, naye akayakata yakawa nyuzi nyembamba ili zifumwe pamoja na zile nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora, akatarizi efodi. **4** Wakatengeneza vipande vya mabegani vilivyunganishwa kwenye miisho yake miwili ya juu. **5** Mshipi uliofumwa unaoshikilia kwa nguvu efodi ulitengenezwa kwa vitu hivyo hivyo,^e yaani, dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

6 Kisha wakatia mawe ya shohamu katika vifuko vya dhahabu na kuchonga majina ya wana wa Israeli kwenye mawe hayo, kama mtu anavyochonga muhuri.^f **7** Akayawe-ka mawe hayo kwenye vipande vya mabegani vya efodi, ili yawe mawe ya ukumbusho

39:2 *Inaelekea ni Bezaleli.

kwa wana wa Israeli,^a kama Yehova alivyomwamuru Musa. **8** Kisha akatengeneza kifuko cha kifuani^b na kukitarizi. Akakitengeneza kama efodi kwa kutumia dhahabu, nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa cha rangi nyekundu, na kitani bora kilichosokotwa.^c **9** Kifuko hicho kilikuwa cha mraba kilipokunjwa mara mbili. Walikitengeneza kifuko hicho cha kifuani kikiwa na urefu wa shubiri moja* na upana wa shubiri moja kinapokunjwa mara mbili. **10** Wakaweka kwenye kifuko hicho mawe yaliyopangwa katika safu nne. Safu ya kwanza ilikuwa na zabarijadi, topazi, na zumaridi. **11** Safu ya pili ilikuwa na feruzi, yakuti, na yaspi. **12** Safu ya tatu ilikuwa na jiwe la *leshemi*,* aki-ki, na amethysti. **13** Safu ya nne ilikuwa na krisolito, shohamu, na yashefi. Mawe hayo yaliwekwa kwenye vifuko vya dhahabu. **14** Yalilingana na majina 12 ya wana wa Israeli, na majina hayo yalichongwa kama muhuri, na kila jina liliwakilisha mojawapo ya makabila 12 ya wana wa Israeli. **15** Kisha wakakitengeneza kifuko cha kifuani minyororo iliyosokotwa, kama kamba za dhahabu safi.^d **16** Halafu wakatengeneza vifuko viwili vya dhahabu na pete mbili za dhahabu na kuzitia kwenye pembe mbili za juu za kifuko hicho. **17** Baada ya hayo wa-

39:9 *Yaani, upana wa kiganja cha mkono kuanzia kidole gumba hadi kidole kidogo, karibu sentimita 22.2 (inchi 8.75). Angalia Nyongeza B14. **39:12** *Jiwe la thamani ambalo halijulikani, huenda ni jiwe la kaharabu, hayasinthi, opali, au tumalini.

SURA YA 39

a Kut 28:12

b Lut 8:8

c Kut 28:15-21

d Kut 28:22-25

Safu ya 2

a Kut 28:26-28

b Kut 28:31-35

katia zile kamba mbili za dhahabu katika pete mbili zilizo kwenye pembe hizo. **18** Kisha wakatia ncha mbili za hizo kamba mbili katika vile vifuko viwili vya mabegani na kuzifunga ncha hizo kwenye vipande viwili vya efodi, sehemu ya mbele. **19** Halafu wakate-
ngeneza pete mbili za dhahabu na kuziweka kwenye pembe mbili za chini, upande wa ndani wa kifuko cha kifuani, upande wa efodi.^a **20** Kisha wakatengeneza pete nyingine mbili za dhahabu upande wa mbele wa efodi, chini ya vipande viwili vya mabegani vya efodi, karibu na mahali inapoungana, juu ya mshipi uliofumwa wa efodi. **21** Hatimaye, wakafunga pete za kifuko cha kifuani pamoja na pete za efodi kwa kamba ya bluu, ili kifuko cha kifuani kibaki mahali pake kwenye efodi, juu ya mshipi uliofumwa, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

22 Kisha akafuma joho lisi-
lo na mikono la efodi kwa nyuzi za bluu peke yake.^b **23** Lili-
likuwa na nafasi ya kupitishia kichwa katikati sehemu ya juu. Sehemu hiyo ilikuwa na ukingo kuizunguka kama wa koti la vita, ili isiraruke. **24** Halafu wakate-
ngeneza kwenye upindo wa joho hilo makomamanga ya nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, na kitambaa cha rangi nyekundu; vitu vyote hivyo vilisokotwa pamoja. **25** Walitengeneza kengele za dhahabu safi na kuzitia kati ya makomamanga kwenye upindo wote wa joho hilo lisilo na mikono; **26** walitia kengele kisha komamanga, kengele kisha komamanga kwenye upi-

ndo wote wa joho hilo lisilo na mikono lililotumiwa kuhudumu, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

27 Pia walifuma kanzu za kitani bora kwa ajili ya Haruni na wanawe,^a **28** na pia kilemba^b cha kitani bora, kofia maridadi za kitani bora,^c suruali fupi*^d za kitani bora kilichosokotwa, **29** na ukumbuu uliofumwa kwa kitani bora kilichosokotwa, nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, na kitambaa cha rangi nyekundu, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

30 Hatimaye, walitengeneza kwa dhahabu safi bamba linalong'aa, yaani, ile ishara takatifu ya wakfu,* na kuchonga maneno haya juu yake kama muhuri unavyochongwa: "Utakatifu ni wa Yehova."^e **31** Wakalifunga bamba hilo kwa kamba ya bluu ili waliweke juu ya kilemba, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

32 Basi wakakamilisha kazi yote ya hema la ibada, yaani, hema la mkutano; Waisraeli walifanya kila jambo ambalo Yehova alimwamuru Musa.^f Hivyo ndivyo walivyofanya.

33 Wakamletea Musa hema la ibada^g pamoja na vifaa vyake vyote: vibanio vyake,^h viuuzi vyake,ⁱ fito zake,^j nguzo zake na vikalio vyake;^k **34** kifuniko chake cha ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu,^l kifuniko chake cha ngozi za sili, na pazia lake;^m **35** sanduku la ushahidi pamoja na fito zakeⁿ na kifuniko chake;^o **36** meza, vyombo vyake vyote^p na mika-

39:28 *Au "nguo za ndani." 39:30 *Au "taji takatifu."

SURA YA 39

a Kut 28:39, 40

b Kut 28:4

c Kut 29:8, 9

d Kut 28:42

e Kut 28:36, 37

Law 8:9

f Kut 25:40

Ebr 8:5

g Kut 36:8

Kut 36:14

h Kut 36:18

i Kut 36:20

j Kut 36:31

k Kut 36:24

l Kut 36:19

m Kut 36:35

n Kut 37:1, 4

o Kut 37:6

p Kut 37:10, 16

Safu ya 2

a Kut 37:17, 23

b Kut 25:38

c Kut 35:27, 28

d Kut 37:25

e Kut 37:29

f Kut 30:34, 35

g Kut 36:37

h Kut 38:1, 4

i Kut 38:6

j Kut 38:30

k Kut 30:18

Kut 38:8

l Kut 38:9-11

m Kut 38:18

n Kut 38:20

o Kut 28:3

p Kut 35:10

Kut 36:1

SURA YA 40

q Hes 7:1

r Kut 25:21

s Hes 4:5

Ebr 9:3

t Kut 26:35

u Kut 25:31

Ebr 9:2

v Kut 25:37

w Kut 30:1

x Kut 26:36

te ya wonyesho; **37** kinara cha taa cha dhahabu safi, taa zake,^a safu zake za taa, na vyombo vyake vyote^b na mafuta kwa ajili ya taa hizo;^c **38** madhabahu^d ya dhahabu, mafuta yanayotumiwa kutia mafuta,^e uvumba uliotiwa manukato,^f pazia la mlango^g wa hema; **39** madhabahu ya shaba^h na wavu wake wa shaba, fito zake,ⁱ vyombo vyake vyote,^j beseni na kinara chake;^k **40** mapazia ya ua yanayoning'inia, nguzo zake na vikalio vyake,^l pazia la mlango^m wa ua, kamba na vingingi vya hemaⁿ na vifaa vyote vya utumishi wa hema la ibada, yaani, hema la mkutano; **41** yale mavazi yaliyofumwa kwa ustadi ya kuhudumu mahali patakatifu, mavazi matakatifu ya kuhani Haruni,^o na mavazi ya wanawe ya kutumikia wakiwa makuhani.

42 Waisraeli walifanya kazi yote kama Yehova alivyomwamuru Musa.^p **43** Musa alipokagua kazi yao yote, aliona kwamba walikuwa wameifanya kama Yehova alivyoamuru; basi Musa akawabariki.

40 Kisha Yehova akamwambia Musa: **2** "Siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza, utajenga hema la ibada, yaani, hema la mkutano.^q **3** Weka sanduku la Ushahidi ndani yake,^r na ulifunike sanduku hilo kwa pazia.^s **4** Ingiza meza^t na upange vyombo vyake juu yake, kisha ulete kinara cha taa^u na kuwasha taa zake.^v **5** Halafu uweke madhabahu ya dhahabu ya kufukizia uvumba^w mbele ya sanduku la Ushahidi na kuweka pazia la mlango wa hema la ibada.^x

6 “Utaweka madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa^a mbele ya mlango wa hema la ibada, yaani, hema la mkutano, 7 na kuweka beseni kati ya hema la mkutano na madhabahu, kisha utie maji ndani ya beseni hilo.^b 8 Halafu utengeneze ua^c kuzunguka hema hilo na kuweka pazia^d kwenye mlango wa ua. 9 Kisha uchukue mafuta yanayotumiwa kutia mafuta^e na kulitia mafuta hema la ibada na vitu vyote vilivyomo,^f nawe ulitakase pamoja na vyombo vyake vyote, ili liwe takatifu. 10 Utatia mafuta madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa pamoja na vyombo vyake vyote na kuitakasa, ili iwe madhabahu takatifu zaidi.^g 11 Nawe ulitie mafuta beseni na kinara chake na kuitakasa.

12 “Kisha mlete Haruni na wanawe karibu na mlango wa hema la mkutano na kuwasha kwa maji.^h 13 Utamvisha Haruni mavazi matakatifuⁱ na kumtia mafuta^j na kumtakasa, naye atanitumikia akiwa kuhani. 14 Baada ya hayo walete wanawe karibu na kuwavisha kanzu.^k 15 Utawatia mafuta kama ulivyomtia mafuta baba yao,^l ili wanitumikie wakiwa makuhani, nao wataendelea kuwa makuhani daima katika vizazi vyao vyote kwa sababu wameitia mafuta.”^m

16 Musa alifanya yote ambayo Yehova alimwamuru.ⁿ Hivyo ndivyo alivyofanya.

17 Katika mwezi wa kwanza, mwaka wa pili, siku ya kwanza ya mwezi, hema la ibada lilitengenezwa.^o 18 Musa alitengeneza hema

SURA YA 40

a Kut 38:1

b Kut 30:18

c Kut 27:9

d Kut 27:16

Kut 38:18

e Kut 30:23-25

f Law 8:10

Hes 7:1

g Kut 29:36, 37

Law 8:11

h Law 8:6

i Kut 29:5

Law 8:7

j Law 8:12

Zb 133:2

k Law 8:13

l Law 8:30

m Ebr 7:11

n Kut 39:43

Kum 4:2

o Hes 7:1

Hes 9:15

Safu ya 2

a Kut 36:24

b Kut 26:15

c Kut 36:31

d Kut 26:7

e Kut 26:14

f Kut 31:18

g Kut 25:22

Kut 37:1

h Kut 37:4

1Fa 8:8

i Kut 37:6

1Nya 28:11

j Law 16:2

k Kut 36:35

Ebr 10:19, 20

l Ebr 9:3

m Kut 37:10

Ebr 9:2

n Kut 25:30

Mt 12:4

o Kut 37:17

p Kut 25:37

Kut 37:23

q Kut 30:1

Kut 37:25

r Kut 30:34, 35

s Kut 30:7

t Kut 26:36

Kut 36:37

u Kut 38:1

v Kut 29:38

la ibada kwa kuweka chini vikatio vyake,^a kuweka viunzi vyake,^b kuweka fito zake,^c na kusimamisha nguzo zake. 19 Akatandaza kitambaa cha hema^d juu ya viunzi vya hema hilo na kuweka kifuniko^e juu yake, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

20 Kisha akachukua yale mabamba ya Ushahidi^f na ku yaweka ndani ya sanduku la Ushahidi,^g akatia fito^h kwenye pete za Sanduku hilo na kuweka kifunikoⁱ juu ya Sanduku hilo.^j 21 Akaingiza sanduku la Ushahidi ndani ya hema la ibada na kuweka pazia^k ambalo lilifunika sanduku la Ushahidi,^l kama Yehova alivyomwamuru Musa.

22 Kisha akaweka meza^m ndani ya hema la mkutano upande wa kaskazini, nje ya pazia, 23 naye akapanga juu yake ile mikateⁿ kwa safu mbele za Yehova, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

24 Akaweka kile kinara cha taa^o ndani ya hema la mkutano mbele ya meza hiyo, upande wa kusini. 25 Kisha akawasha zile taa^p mbele za Yehova, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

26 Halafu akaweka ile madhabahu ya dhahabu^q ndani ya hema la mkutano mbele ya pazia, 27 ili afukize juu yake uvumba^r uliotiwa manukato,^s kama Yehova alivyomwamuru Musa.

28 Kisha akaweka pazia^t la mlango wa hema la ibada.

29 Akaweka madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa^u kwenye mlango wa hema la ibada, yaani, hema la mkutano, ili atoe juu yake dhabihu za kuteketezwa^v na matoleo ya

nafaka, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

30 Kisha akaweka beseni kati ya hema la mkutano na madhabahu na kutia maji ndani yake ili makuhani wanawe^a mikono na miguu yao.

31 Musa na pia Haruni na wanawe walitumia maji ya beseni hilo kunawa mikono na miguu yao. **32** Kila mara walipoenda kwenye hema la mkutano au kukaribia madhabahu, walinawa^b mikono na miguu yao, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

33 Mwishowe akatengeneza ua^c kuzunguka hema la ibada na ile madhabahu na kuweka pazia la mlango wa ua.^d

Basi Musa akakamilisha kazi yote. **34** Ndipo wingu likaa-

SURA YA 40

a Kut 30:18

b Kut 30:18, 19

c Kut 27:9
Kut 38:9

d Kut 38:18

Safu ya 2

a Hes 9:15
Ufu 15:8

b 2Nya 5:14

c Hes 10:11
Ne 9:19

d Hes 9:17, 22

e Kut 13:21
Hes 9:16
Zb 78:14

na nza kufunika hema la mku-tano, na utukufu wa Yehova ukajaa katika hema la ibada.^a

35 Musa alishindwa kuingia ndani ya hema la mkutano kwa sababu wingu liliendelea kulifunika, na utukufu wa Yehova ukajaa katika hema hilo.^b

36 Kila mara wingu lilipoinuka kutoka juu ya hema la ibada, Waisraeli walivunja kambi katika hatua zote za safari yao.^c **37** Hata hivyo, wingu lilipokosa kuinuka, hawakuvunja kambi mpaka siku lilipoinuka.^d **38** Katika hatua zote za safari yao, Waisraeli wote waliona wingu la Yehova likiwa juu ya hema la ibada wakati wa mchana, na moto ukiwa juu yake wakati wa usiku.^e

MAMBO YA WALAWI

YALIYOMO

- | | | | | |
|---|--|--|----|--|
| 1 | Dhabihu ya kuteketezwa (1-17) | | 7 | Maagizo kuhusu dhabihu (1-21)
Dhabihu ya hatia (1-10)
Dhabihu ya ushirika (11-21)
Wakatazwa kula mafuta au damu (22-27)
Fungu la kuhani (28-36)
Orodha ya dhabihu mbalimbali (37, 38) |
| 2 | Toleo la nafaka (1-16) | | 8 | Haruni na wanawe wawekwa rasmi kuwa makuhani (1-36) |
| 3 | Dhabihu ya ushirika (1-17)
Msile mafuta wala damu (17) | | 9 | Haruni atoa dhabihu (1-24) |
| 4 | Dhabihu ya dhambi (1-35) | | 10 | Moto kutoka kwa Yehova wawaangamiza Nadabu na Abihu (1-7)
Sheria ya makuhani kuhusu kula na kunywa (8-20) |
| 5 | Dhambi hususa na dhabihu zilizohitaji kutolewa (1-6)
Kutoa habari kuhusu dhambi za wengine (1)
Dhabihu ambazo zingeweza kutolewa na maskini (7-13)
Dhabihu ya hatia kwa ajili ya dhambi zilizotendwa bila kukusudia (14-19) | | 11 | Wanyama safi na wasio safi (1-47) |
| 6 | Habari zaidi kuhusu dhabihu ya hatia (1-7)
Maagizo kuhusu dhabihu (8-30)
Dhabihu ya kuteketezwa (8-13) | | | |

- 12 Kutakaswa kwa mwanamke baada ya kuzaa mtoto (1-8)
- 13 Sheria kuhusu ukoma (1-46)
Ukoma unaoathiri mavazi (47-59)
- 14 Kujitakasa ukoma (1-32)
Kutakasa nyumba zilizoathiriwa (33-57)
- 15 Umajimaji unaotoka kwenye viungo vya uzazi (1-33)
- 16 Siku ya Kufunika Dhambi (1-34)
- 17 Hema la ibada, mahali pa kutoa dhabihu (1-9)
Wakatazwa kula damu (10-14)
Sheria kuhusu wanyama waliokufa (15, 16)
- 18 Ngono haramu (1-30)
Msiwaige Wakanaani (3)
Ngono mbalimbali kati ya watu wa ukoo (6-18)
Wakati wa hedhi (19)
Ngono kati ya watu wa jinsia moja (22)
Ngono na wanyama (23)
'Msijichafue, kama sivyo, nchi itawatapika' (24-30)
- 19 Sheria mbalimbali kuhusu utakatifu (1-37)
Njia inayofaa ya kuvuna (9, 10)
Kuwajibaji viziwi na vipofu (14)
Uchongezi (16)
Usiwe na kinyongo (18)
Wakatazwa kufanya uchawi na kuwasiliana na roho waovu (26, 31)
Wakatazwa kuchanja chale (28)
Kuwaheshimu waliozeeka (32)
Jinsi wageni wanavyopaswa kutendewa (33, 34)
- 20 Ibada ya Moleki; kuwasiliana na roho waovu (1-6)
Iweni watakatifu na muwaheshimu wazazi (7-9)
Wanaofanya ngono haramu wanapaswa kuuawa (10-21)
Iweni watakatifu ili mwendeele kuishi nchini (22-26)
Wanaowasiliana na roho waovu wanapaswa kuuawa (27)
- 21 Makuhani wawe watakatifu, wasiwe wachafu (1-9)
- Kuhani mkuu asijichafue (10-15)
Makuhani wasiwe na kasoro yoyote mwilini (16-24)
- 22 Utakatifu wa makuhani na ulaji wa vitu vitakatifu (1-16)
Dhabihu zisizo na kasoro ndizo zinazokubaliwa (17-33)
- 23 Siku takatifu na sherehe takatifu (1-44)
Sabato (3)
Pasaka (4, 5)
Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu (6-8)
Kutoa mazao au matunda ya kwanza (9-14)
Sherehe ya Majuma (15-21)
Njia inayofaa ya kuvuna (22)
Sherehe ya Kupiga Tarumbeta (23-25)
Siku ya Kufunika Dhambi (26-32)
Sherehe ya Vibanda (33-43)
- 24 Mafuta kwa ajili ya taa za hema la ibada (1-4)
Mikate ya wonyesho (5-9)
Aliyelitukana jina la Mungu apigwa mawe (10-23)
- 25 Mwaka wa Sabato (1-7)
Mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50 (8-22)
Kurudishwa kwa mali (23-34)
Jinsi ya kuwatendea maskini (35-38)
Sheria kuhusu utumwa (39-55)
- 26 Epukeni ibada ya sanamu (1, 2)
Baraka za kuwa mtiifu (3-13)
Adhabu ya kukosa kutii (14-46)
- 27 Kukomboa vitu vilivyowekwa nadhiri (1-27)
Watu (1-8)
Wanyama (9-13)
Nyumba (14, 15)
Mashamba (16-25)
Mzaliwa wa kwanza (26, 27)
Vitu vilivyotolewa kwa Yehova bila masharti (28, 29)
Kukomboa sehemu za kumi (30-34)

1 Na Yehova akamwita Musa na kuzungumza naye kati-ka hema la mkutano,^a akamwambia: **2** “Zungumza na Waisraeli* uwaambie, ‘Ikiwa yeyote kati yenu atamtolea Yehova mnyama wa kufugwa, anapaswa kumtolea dhabihu kutoka kati ya mifugo yake au kundi lake.^b

3 “Ikiwa anatoa dhabihu ya kuteketezwa kutoka kati ya mifugo yake, anapaswa kutoa mnyama dume asiye na kasoro.^c Atamtoa kwa hiari yake mwenyewe^d mbele za Yehova kwenye mlango wa hema la mkutano. **4** Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha dhabihu hiyo ya kuteketezwa, nayo itakubaliwa kwa niaba yake ili kufunika dhambi zake.

5 “Kisha huyo ng’ombe dume mchanga atachinjwa mbele za Yehova, nao wana wa Haruni, makuhani,^e wataleta damu ya mnyama huyo na kuinyunyiza pande zote za madhabahu,^f kwenye mlango wa hema la mkutano. **6** Mnyama huyo wa dhabihu ya kuteketezwa anapaswa kuchunwa ngozi na kukatwa vipandevipande.^g **7** Wana wa Haruni, makuhani, wataweka moto kwenye madhabahu^h na kupanga kuni kwenye moto huo. **8** Wana wa Haruni, makuhani, watapanga vile vipande vya mnyama wa dhabihuⁱ pamoja na kichwa na mafuta yanayofunika figo juu ya kuni kwenye moto wa madhabahu. **9** Matumbo na miguu yake itaoshwa kwa maji, na kuhani atachoma moto vitu hivyo vyote ili vifuke moshi kwenye madhabahu. Ni dha-

SURA YA 1

a Kut 40:34

b Law 22:18-20

c Kum 15:19, 21
Mal 1:14

d 2Ko 9:7

e Ebr 10:11

f Ebr 9:13, 14

g Law 7:8

h Law 6:12

i 1Fa 18:23

Safu ya 2

a Mwa 8:20, 21
Hes 15:2, 3

b Mwa 4:4

c Law 12:6
Law 22:18-20

d Kut 29:16-18
Law 8:18-21
Law 9:12-14

e Law 5:7
Law 12:8
Lu 2:24

bihi ya kuteketezwa, dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.^a

10 “Ikiwa anatoa dhabihu kutoka katika kundi,^b yaani, kutoka kati ya wana-kondoo dume au mbuzi, anapaswa kutoa dume asiye na kasoro.^c **11** Atachinjwa upande wa kaskazini wa madhabahu mbele za Yehova, nao wana wa Haruni, makuhani, watanyunyiza damu yake pande zote za madhabahu.^d **12** Atamkata vipandevipande, naye kuhani atavipanga vipande hivyo pamoja na kichwa na mafuta yaliyo kwenye figo juu ya kuni kwenye moto wa madhabahu. **13** Ataosha matumbo na miguu yake kwa maji, kisha kuhani atavileta vyote na kuvichoma moto ili vifuke moshi kwenye madhabahu. Ni dhabihu ya kuteketezwa, dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.

14 “Hata hivyo, ikiwa anamtoa ndege kuwa dhabihu ya kuteketezwa kwa Yehova, atamtoa njiwa tetere au hua mchanga.^e **15** Kuhani atamtoa kwenye madhabahu, atamvunja shingo na kuacha kichwa kikining’inia, kisha atamchoma moto juu ya madhabahu ili afuke moshi, lakini damu yake itamwagwa kando ya madhabahu. **16** Ataondoa kifuko cha chakula kilicho kooni mwake pamoja na manyoya yake na kuvitupa vitu hivyo kando ya madhabahu, upande wa mashariki,

1:2 *Tnn., “wana wa Israeli.”

1:9, 13 *Au “inayomtuliza.”

mahali panapowekwa majivu.*^a **17** Atampasua kwenye mabawa yake bila kumkata vipande viwili. Kisha kuhani atamchoma moto juu ya kuni zilizo kwenye madhabahu ili afuke moshi. Ni dhabihu ya kuteketezwa, dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.

2 “Sasa ikiwa mtu atamotolea Yehova toleo la nafaka,^b ni lazima toleo lake liwe la unga laini, naye anapaswa kumimina mafuta juu yake na kuweka ubani juu yake.^c **2** Kisha atalipeleka kwa wana wa Haruni, makuhani, naye kuhani atachukua mkono mmoja wa unga huo laini, mafuta, pamoja na ubani wake wote, naye atauteketeza ili ufuke moshi ikiwa dhabihu ya kumbukumbu^d juu ya madhabahu. Ni dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova. **3** Chochote kinachobaki cha toleo hilo la nafaka kitakuwa cha Haruni na wanawe,^e kitakuwa kitu kitakatifu kabisa^f kutoka kwa dhabihu za Yehova zinazochomwa kwa moto.

4 “Mkitoa nafaka ambayo imeokwa kwenye jiko, inapaswa kuwa ya unga laini, mikate ya mvingo isiyo na chachu na iliyokandwa kwa mafuta, au mikate myembamba isiyo na chachu ambayo imepakwa mafuta.^g

5 “Mkitoa toleo la nafaka kutoka katika kiokeo,^h inapaswa kuwa ya unga laini usio na chachu, uliokandwa kwa

1:16 *Au “majivu yenye mafuta,” yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhabihu. 1:17; 2:2, 9 *Au “inayomtuliza.” 2:2, 9 #Au “ikiwa sehemu ya ukumbusho (uwa-kilishi) wake.”

SURA YA 1

a Kut 27:3
Law 4:11,12
Law 6:10

SURA YA 2

b Law 9:17
Hes 15:2-4

c Kut 29:1-3
Law 6:14,15
Hes 7:13

d Hes 5:25, 26

e Law 7:9,10

f Law 10:12
Hes 18:9

g Law 8:26, 28
Hes 6:13, 19

h Law 6:20, 21

Safu ya 2

a Hes 28:9

b Law 2:2
Law 5:11,12

c Kut 29:38-41
Hes 28:4-6

d Hes 18:9

e Law 6:14,17

f Kut 23:19
Hes 15:20
2Nya 31:5
Met 3:9

mafuta. **6** Toleo hilo litavunjwa vipandevipande na mafuta yatamiminwa juu yake.^a Ni toleo la nafaka.

7 “Mkitoa toleo la nafaka iliyokaangwa kwenye kikaa-ngio, linapaswa kuwa la unga laini uliokandwa kwa mafuta. **8** Mnapaswa kumletea Yehova toleo la nafaka lililotengenezwa kwa vitu hivyo, nalo litapelekwa kwa kuhani ambaye atalipeleka karibu na madhabahu. **9** Naye kuhani atachukua sehemu ya toleo hilo la nafaka ikiwa dhabihu ya kumbukumbu^b na kuiteketeza juu ya madhabahu ili ifuke moshi. Ni dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.^c **10** Chochote kinachobaki cha toleo hilo la nafaka kitakuwa cha Haruni na wanawe, kitakuwa kitu kitakatifu kabisa kutoka kwa dhabihu za Yehova zinazoteketezwa.^d

11 “Toleo lolote la nafaka mnalomtolea Yehova halipaswi kutiwa chachu,^e kwa maana hampaswi kuuteketeza unga wowote uliokandwa ulio na chachu au kuiteketeza asali ili ifuke moshi ikiwa toleo la Yehova linalochomwa kwa moto.

12 “Mnaweza kumtolea Yehova vitu hivyo vikiwa mazao ya kwanza,^f lakini hampaswi kuvileta kwenye madhabahu vikiwa dhabihu ya kuteketezwa yenye harufu inayompendeza.*

13 “Kila toleo la nafaka mnalotoa linapaswa kukolezwa kwa chumvi; na msiruhusu kamwe chumvi ya agano la Mungu wenu ikosekane kati-

2:12 *Au “inayotuliza.”

ka toleo lenu la nafaka. Kila toleo mtakalotoa, mtalitoa pamoja na chumvi.^a

14 “Mkimtolea Yehova mavuno ya kwanza ya nafaka iliyokoma yakiwa toleo la nafaka, mnapaswa kutoa masuke mabichi yaliyokaangwa kwa moto, chengachenga za nafaka mbichi iliyopondwa, kuwa toleo la nafaka la mavuno yenu ya kwanza yaliyokomaa.^b

15 Mnapaswa kutia mafuta na ubani juu yake. Ni toleo la nafaka. **16** Kuhani ataiteke-teza ikiwa dhabihu ya kumbu-kumbu*^c ili ifuke moshi, yaani, baadhi ya chengachenga za nafaka pamoja na mafuta na ubani wake wote. Ni dhabihu kwa Yehova inayocho-mwa kwa moto.

3 “Ikiwa mtu anatoa dhabihu ya ushirika*^d na dhabihu hiyo inatoka kati ya mifugo, awe ni mnyama dume au jike, anapaswa kumtolea Yehova mnyama asiye na kasoro. **2** Anapaswa kuweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama huyo, naye atachinjwa kwenye mlango wa hema la mkutano; kisha wana wa Haruni, makuhani, watanyunyiza damu yake pande zote za madhabahu. **3** Atatoa sehemu ya dhabihu hiyo ya ushirika kuwa dhabihu kwa Yehova^e inayocho-mwa kwa moto, yaani, mafuta^f yanayofunika matumbo, naam, mafuta yote yaliyo juu ya matumbo, **4** na figo zake mbili pamoja na mafuta yake yaliyo karibu na kiuno. Ataondoa pia figo pamoja na mafuta yaliyo juu ya ini.^g

2:16 *Au “ikiwa sehemu ya ukumbusho (uwakilishi) wake.” 3:1 *Au “dhabihu ya matoleo ya amani.”

SURA YA 2

a Eze 43:23, 24

b Kut 23:16
Kut 34:22
Hes 28:26c Law 5:11, 12
Law 6:14, 15

SURA YA 3

d Law 22:21
Hes 6:13, 14

e Law 7:29-31

f Kut 29:13
Law 7:23-25
1Fa 8:64

g Law 7:1-4

Safu ya 2

a Law 6:12

b Law 4:29, 31

c Hes 6:13, 14

d Kut 29:22
Law 9:18-20
2Nya 7:7e Law 4:8, 9
Law 9:10

f Law 4:31

MAMBO YA WALAWI 2:14-3:13

5 Wana wa Haruni watateke-teza vitu hivyo kwenye madhabahu juu ya dhabihu ya kuteketezwa iliyo kwenye kuni zinazowaka moto ili vifuke moshi;^a ni dhabihu inayocho-mwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.^b

6 “Ikiwa mtu anamtolea Yehova dhabihu ya ushirika kutoka kati ya kundi lake, anapaswa kutoa mnyama dume au jike asiye na kasoro.^c

7 Ikiwa anatoa kondoo dume mchanga, atamtoa mbele za Yehova. **8** Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama huyo, naye atachinjwa mbele ya hema la mkutano. Kisha wana wa Haruni, makuhani, watanyunyiza damu yake pande zote za madhabahu. **9** Atayatoa mafuta kutoka kwenye dhabihu ya ushirika yawe dhabihu kwa Yehova inayocho-mwa kwa moto.^d Atakata mkia wote wenye mafuta karibu na uti wa mgongo, ataondoa mafuta yanayofunika matumbo, naam, mafuta yote yaliyo juu ya matumbo, **10** na figo zake mbili pamoja na mafuta yake yaliyo karibu na kiuno. Ataondoa pia figo pamoja na mafuta yaliyo juu ya ini.^e **11** Naye kuhani ataviteketeza vitu hivyo kwenye madhabahu kama chakula* ili vifuke moshi. Ni dhabihu kwa Yehova inayocho-mwa kwa moto.^f

12 “Ikiwa mtu anatoa mbuzi, atamtoa mbele za Yehova. **13** Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha mbuzi huyo, naye atachinjwa mbele

3:5 *Au “inayomtuliza.” 3:11 *Tnn., “mkate,” yaani, sehemu ya Mungu ya dhabihu ya ushirika.

ya hema la mkutano, nao wana wa Haruni watanyunyiza damu yake pande zote za madhabahu. **14** Atamtolea Yehova mafuta yanayofunika matumbo, naam, mafuta yote yaliyo juu ya matumbo kuwa dhabihu inayocho-mwa kwa moto,^a **15** pamoja na figo zake mbili na mafuta yake yaliyo karibu na kiuno. Ataondoa pia figo pamoja na mafuta yaliyo juu ya ini. **16** Kuhani atavitekeza vitu hivyo kwenye madhabahu kama chakula* ili vifuke moshi, ni dhabihu inayocho-mwa kwa moto yenye harufu inayopendeza.[#] Mafuta yote ni ya Yehova.^b

17 “Ni sheria ya kudumu kwa vizazi vyenu, katika makao yenu yote: Msile mafuta yoyote wala damu^c yoyote.”

4 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Waabie Waisraeli, ‘Mtu akitenda dhambi bila kukusudia^d kwa kufanya jambo lolote ambalo Yehova ameamuru lisifanywe:

3 “Kuhani aliyetiwa mafuta^e akitenda dhambi^f na kuwaletea watu hatia, basi atamtolea Yehova ng’ombe dume mchanga asiye na kaso-ro, kuwa dhabihu ya dhambi kwa ajili ya dhambi aliyotenda.^g **4** Atamleta huyo ng’ombe dume kwenye mlango wa hema la mkutano^h mbele za Yehova na kuweka mko-no wake juu ya kichwa cha ng’ombe dume huyo, naye atamchinja mbele za Yehova.ⁱ **5** Kisha kuhani aliyetiwa mafuta^j atachukua kiasi

3:16 *Tnn., “mkate,” yaani, sehemu ya Mungu ya dhabihu ya ushirika. [#]Au “inayotuliza.”

SURA YA 3

a Law 4:24, 26

b Law 7:23

1Sa 2:15-17

c Mwa 9:4

Law 17:10, 13

Kum 12:23

Mdo 15:20, 29

SURA YA 4

d Law 5:17

Hes 15:27, 28

e Law 8:12

Law 21:10

f Hes 12:1, 11

g Ebr 5:1-3

Ebr 7:27

h Law 6:25

i Kut 29:10, 11

j Kut 30:30

Safu ya 2

a Law 8:15, 16

b Law 16:14, 19

c Kut 30:10

d Law 5:9

e Law 9:8, 10

f Law 3:3, 4

g Kut 29:14

h Law 8:14, 17

Ebr 13:11

fulani cha damu ya ng’ombe dume huyo na kuileta ndani ya hema la mkutano; **6** naye atachovya kidole chake ndani ya damu^a hiyo na kunyunyiza kiasi fulani mara saba^b mbele za Yehova, mbele ya pazia la mahali patakatifu. **7** Pia, kuhani atatia kiasi fulani cha damu hiyo kwenye pembe za madhabahu ya uvumba uliotiwa manukato,^c mbele za Yehova katika hema la mkutano; naye atamwaga damu yote ili-yobaki ya huyo ng’ombe dume kwenye msingi wa madhabahu ya dhabihu za kute-ketezwa,^d kwenye mlango wa hema la mkutano.

8 “Kisha ataondoa mafuta yote ya huyo ng’ombe dume wa dhabihu ya dhambi, pamoja na mafuta yanayofunika matumbo na mafuta yanayo-zunguka matumbo, **9** na figo zake mbili pamoja na mafuta yake yaliyo karibu na kiuno. Ataondoa pia figo pamoja na mafuta yaliyo juu ya ini.^e **10** Ataondoa sehemu zilezile zinazoondolewa katika ng’ombe dume wa dhabihu ya ushirika.^f Na kuhani atavitekeza kwenye madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa ili vifuke moshi.

11 “Lakini ngozi ya ng’ombe dume huyo na nyama yake yote pamoja na kichwa chake, miguu yake, matumbo yake, na mavi yake^g— **12** sehemu zote zinazobaki za ng’ombe dume huyo—atazipeleka mahali safi nje ya kambi, mahali ambapo majivu* hutupwa, naye atazitekeza kwa moto juu ya kuni.^h Zinapaswa

4:12 *Au “majivu yenye mafuta,” yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhabihu.

kuteketezwa mahali ambapo majivu hutupwa.

13 “Sasa ikiwa kusanyiko lote la Waisraeli lina hatia ya kutenda dhambi bila kukusudia,^a lakini halikujua kwamba limefanya jambo ambalo Yehova aliamuru lisifanywe,^b

14 kisha dhambi hiyo ijulikane, ni lazima kusanyiko litoe ng’ombe dume mchanga kwa ajili ya dhabihu ya dhambi na kumleta mbele ya hema la mkutano. **15** Wazee wa kusanyiko hilo wataweka mikono yao juu ya kichwa cha ng’ombe dume huyo mbele za Yehova, naye atachinjwa mbele za Yehova.

16 “Kisha kuhani aliyetiwa mafuta ataleta kiasi fulani cha damu ya ng’ombe dume huyo katika hema la mkutano. **17** Naye atachovya kidole chake ndani ya damu hiyo na kunyunyiza kiasi fulani mara saba mbele za Yehova, mbele ya pazia.^c **18** Kisha atatia kiasi fulani cha damu hiyo kwenye pembe za madhabahu^d iliyo mbele za Yehova, katika hema la mkutano; naye atamwaga damu yote iliyobaki kwenye msingi wa madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa, iliyo kwenye mlango wa hema la mkutano.^e **19** Atandoa mafuta yake yote na kuyateketeza kwenye madhabahu ili yafuke moshi.^f **20** Atamfanya ng’ombe dume huyo kama alivyomfanya yule ng’ombe dume wa dhabihu ya dhambi. Hivyo ndivyo atakavyomfanya, kuhani atatoa dhabihu ya kufunika dhambi zao,^g nao watasamehewa. **21** Atampeleka ng’ombe dume huyo nje ya kambi na kumtekeza kama alivyomtekeza ng’o-

SURA YA 4

a Yos 7:11

b Hes 15:22-24

c Kut 26:31
Kut 40:21
Ebr 10:19, 20

d Kut 30:1, 6

e Kut 27:1
Kut 40:6

f Law 3:16

g Kut 32:30
Law 16:17
Hes 15:25
Efe 1:7
Ebr 2:17

Safu ya 2

a Law 4:11, 12

b Law 16:15
1Yo 2:1, 2

c Kut 18:21

d Law 1:10, 11
Law 6:25
Law 7:2

e Law 9:8, 9
Law 16:18
Ebr 9:22

f Law 8:15

g Law 3:3-5

h Hes 15:27-29

mbe dume wa kwanza.^a Ni dhabihu ya dhambi kwa ajili ya kusanyiko lote.^b

22 “Ikiwa mkuu^c ametenda dhambi bila kukusudia na hivyo ana hatia ya kufanya jambo lolote ambalo Yehova Mungu wake ameamuru lisifanywe, **23** au akigundua dhambi aliyotenda kinyume cha amri, basi anapaswa kumleta mwanambuzi dume asiye na kasoro ili atolewe dhabihu kwa ajili yake. **24** Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha mwanambuzi huyo na kumchinja mahali ambapo dhabihu za kuteketezwa huchinjwa mbele za Yehova.^d Hiyo ni dhabihu ya dhambi. **25** Kuhani atachukua kwa kidole chake kiasi kidogo cha damu ya dhabihu ya dhambi na kuitia kwenye pembe^e za madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa, naye atamwaga damu inayobaki kwenye msingi wa madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa.^f **26** Naye atayateketeza mafuta yake yote kwenye madhabahu ili yafuke moshi kama yale mafuta ya dhabihu ya ushirika;^g naye kuhani atatoa dhabihu ya kufunika dhambi ya mtu huyo, naye atasamehewa.

27 “Mtu yeyote miongoni mwa watu walio nchini akienda dhambi bila kukusudia na hivyo kuwa na hatia ya kufanya jambo lolote ambalo Yehova ameamuru lisifanywe,^h **28** au akigundua dhambi aliyotenda, basi atamleta mwanambuzi jike asiye na kasoro ili atolewe dhabihu kwa ajili ya dhambi aliyotenda. **29** Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama

wa dhabihu ya dhambi na kumchinjia mahali ambapo dhambihu za kuteketezwa huchinjwa.^a **30** Kuhani atachukua kwa kidole chake kiasi kidogo cha damu ya mnyama huyo na kuitia kwenye pembe za madhabahu ya dhambihu za kuteketezwa, naye atamwaga damu yote inayobaki kwenye msingi wa madhabahu.^b **31** Ataondoa mafuta yake yote^c kama mafuta ya dhambihu ya ushirika^d yanavyoondolewa, na kuhani atayateketeza kwenye madhabahu ili yafuke moshi yakiwa harufu inayompendeza* Yehova; naye kuhani atatoa dhambihu ya kufunika dhambi ya mtu huyo, naye atasamehewa.

32 “Lakini akitoa mwanakondoo ili awe dhambihu yake ya dhambi, anapaswa kuleta mwanakondoo jike asiye na kasoro. **33** Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama wa dhambihu ya dhambi na kumchinjia mahali ambapo dhambihu za kuteketezwa huchinjwa.^e **34** Kuhani atachukua kwa kidole chake kiasi kidogo cha damu ya mnyama huyo na kuitia kwenye pembe za madhabahu ya dhambihu za kuteketezwa,^f naye atamwaga damu yote inayobaki kwenye msingi wa madhabahu. **35** Ataondoa mafuta yake yote kama mafuta ya mwanakondoo dume wa dhambihu ya ushirika yanavyoondolewa, na kuhani atayateketeza kwenye madhabahu juu ya dhambihu za Yehova zinazochomwa kwa moto;^g naye kuhani atatoa dhambihu ya kufunika dhambi ambayo mtu huyo alitenda, naye atasamehewa.^h

4:31 *Au “inayomtuliza.”

SURA YA 4

a Law 1:10, 11
Law 6:25

b Law 4:25
Law 8:15
Law 9:8, 9
Ebr 9:22

c Law 3:16

d Law 3:3, 4

e Law 1:10, 11

f Law 4:25
Law 16:18

g Kut 29:13, 14
Law 3:3, 4
Law 6:12
Law 9:8, 10

h Hes 15:28
1Yo 1:7
1Yo 2:1, 2

Safu ya 2

SURA YA 5

a Met 29:24

b Law 11:21-24
Law 17:15
Kum 14:8

c Law 12:2
Law 13:3
Law 15:3
Hes 19:11

d Mt 5:33

e Hes 5:7
Zb 32:5
Met 28:13
1Yo 1:9

f Law 7:1
Law 14:2, 12
Law 19:20, 21
Hes 6:12

5 “Ikiwa mtu amesikia mwito wa hadharani wa kutoa ushahidi*^a kuhusu jambo ambalo amejionea au kusikia au kujua, lakini amekataa kutoa habari, basi ametenda dhambi, naye atawajibika kwa sababu ya kosa lake.

2 “Au mtu akigusa kitu chochote kisicho safi, iwe ni mzoga wa mnyama wa mwituni, mzoga wa mnyama wa kufugwa, au viumbe wanaoishi katika makundi makubwa,^b hatakuwa safi na atakuwa na hatia hata kama hajui jambo hilo. **3** Au mtu akigusa uchafu wa mwanadamu bila kujua^c—kitu chochote kisicho safi kinachoweza kumchafua—atakuwa na hatia atakapojua jambo hilo.

4 “Au mtu akiapa kufanya jambo fulani bila kufikiri—jambo lolote lile, jema au baya—lakini baadaye atambue kwamba ameapa bila kufikiri, atakuwa na hatia atakapojua jambo hilo.*^d

5 “Ikiwa ana hatia katika jambo lolote kati ya mambo hayo, basi ni lazima aungame^e dhambi aliyotenda. **6** Pia atamletea Yehova dhambihu ya hatia kwa ajili ya dhambi aliyotenda;^f ataleta mnyama jike kutoka katika kundi, yaani, mwanakondoo jike au mwanambuzi jike, ili awe dhambihu ya dhambi. Kisha kuhani atamtolea dhambihu ya kufunika dhambi yake.

7 “Hata hivyo, ikiwa hawazi kutoa kondoo, atamletea

5:1 *Tnn., “amesikia laana (kiapo).” Labda anasikia tangazo kuhusu kosa lililofanywa na laana itakayompata mko-saji au shahidi yeyote anayekataa kutoa ushahidi. 5:4 *Inaonekana mtu huyo hatimizi kiapo chake.

Yehova njiwa tetere wawili au hua wawili wachanga^a wawe dhabihu ya hatia kwa ajili ya dhambi yake, ndege mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, na mwingine kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa.^b **8** Atawaleta kwa kuhani, naye kuhani atatoa ndege mmoja kwanza kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, atamvunja shingo na kuacha kichwa kikining'inia. **9** Atanyunyiza kiasi kidogo cha damu ya dhabihu hiyo ya dhambi kando ya madhabahu, lakini damu inayobaki itamwagwa kwenye msingi wa madhabahu.^c Ni dhabihu ya dhambi. **10** Atamtóa ndege wa pili kuwa dhabihu ya kuteketezwa akifuata utaratibu wa kawaida;^d naye kuhani atamtólea dhabihu ya kufunika dhambi aliyotenda, naye atasamehewa.^e

11 “Ikiwa hawezi kutoa njiwa tetere wawili au hua wawili wachanga, basi atatoa sehemu ya kumi ya kipimo cha efa moja^{*f} ya unga laini ili kuwa dhabihu ya dhambi. Hapaswi kuutia mafuta au ubani kwa sababu ni dhabihu ya dhambi. **12** Atauleta kwa kuhani, naye kuhani atachukua mkono mmoja wa unga huo ukiwa dhabihu ya kumbukumbu* naye atauweka kwenye madhabahu juu ya dhabihu za Yehova zinazochomwa kwa moto ili ufuke moshi. Ni dhabihu ya dhambi. **13** Kuhani atamtólea dhabihu ya kufunika dhambi aliyot-

5:11 *Sehemu ya kumi ya efa ilikuwa sawa na lita 2.2 au kilogramu 1.3 hivi. Angalia Nyongeza B14. 5:12 *Au “ukiwa sehemu ya ukumbusho (uwakilishi) wake.”

SURA YA 5

a Lu 2:24

b Law 12:7,8
Law 14:21, 22
Law 15:13-15c Law 1:4, 5
Law 7:2
Ebr 9:22

d Law 1:15-17

e Law 6:7

f Kut 16:36

Safu ya 2

a Law 4:26

b Law 2:10
Law 7:1, 6c Law 6:14-16
1Ko 9:13

d Law 10:17, 18

e Law 6:6

f Kut 30:13
Law 27:25g Law 6:4, 5
Law 22:14
Hes 5:6, 7

h Kut 32:30

i Law 6:7
Law 19:22

j Law 5:2

k Law 6:6

tenda, yoyote kati ya dhambi hizo, naye atasamehewa.^a Sehemu inayobaki ya dhabihu hiyo itakuwa ya kuhani,^b sawa na sehemu inayobaki ya toleo la nafaka.”^c

14 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **15** “Mtu akikosa uaminifu kwa kute nda dhambi bila kukusudia kwa kuvunja sheria kuhusu vitu vitakatifu vya Yehova,^d anapaswa kumletea Yehova kondoo dume asiye na kasoro kutoka kundini ili awe dhabihu ya hatia;^e thamani yake itapimwa kwa shekeli za fedha* kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.”^f

16 Naye atalipia dhambi aliyotenda dhidi ya mahali patakatifu na pia ataongeza sehemu ya tano ya thamani ya vitu hivyo.^g Atampa kuhani, ili kuhani amtolee dhabihu ya kufunika dhambi^h yake akitumia kondoo dume wa dhabihu ya hatia, naye atasamehewa.ⁱ

17 “Mtu akitenda dhambi kwa kufanya jambo lolote ambalo Yehova ameamuru lisifanywe, hata kama hajui, bado ana hatia naye atawajibika kwa sababu ya kosa lake.^j **18** Anapaswa kumletea kuhani kondoo dume asiye na kasoro kutoka kundini kulingana na thamani iliyokadiriwa, kwa ajili ya dhabihu ya hatia.^k Kisha kuhani atamtólea dhabihu ya kufunika kosa alilofanya bila kukusudia na bila kujua, naye atasamehewa. **19** Ni dhabihu ya hatia. Bila shaka ana hatia ya kumtendea dhambi Yehova.”

5:15 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. ^aAu “shekeli takatifu.”

6 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Mtu akitenda dhambi na kukosa uaminifu kwa Yehova^a kwa kumdanganya jirani yake kuhusu kitu fulani alichokabidhiwa atunze,^b au alichochiwa kama dhamana, au akimwibia au kumlaghai jirani yake, **3** au akipata kitu kilichopotea na kudanganya kwamba hajakipata, naye akiapa kwa uwongo kuhusu dhambi yoyote kama hiyo ambayo hue nda akatenda,^c anapaswa kufanya hivi: **4** Ikiwa ametenda dhambi naye ana hatia, ni lazima arudishe kitu alichoiwa, kitu alichochukua kwa nguvu, kitu alichochukua kwa ulaghai, kitu alichokabidhiwa atunze, au kitu kilichopotea akakipata, **5** au chochote alichopata kwa uwongo, ni lazima alipe kitu hicho kikamili^d na kuongeza sehemu ya tano ya thamani yake. Atamrudishia mwenyewe kitu hicho siku ambayo hatia yake itajulikana. **6** Naye atamletea kuhani kondoo dume asiye na kasoro kutoka kundini ili amtolee Yehova dhabihu ya hatia kulingana na thamani iliyokadiriwa ya dhabihu ya hatia.^e **7** Kuhani atamtolea dhabihu ya kufunika dhambi yake mbele za Yehova, naye atasamehe wa kosa lolote ambalo lilifanya awe na hatia.”^f

8 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **9** “Mwamuru hivi Haruni na wanawe: ‘Hii ndiyo sheria kuhusu dhabihu ya kuteketezwa:^g Dhabihu ya kuteketezwa itakaa usiku kucha motoni juu ya madhabahu mpaka asubuhi, hakikisheni kwamba moto wa madhabahu unaendelea kuwaka. **10** Ku-

SURA YA 6

a Hes 5:6

b Kut 22:7
Law 19:11c Kut 22:10, 11
Law 19:12
Efe 4:25
Kol 3:9d Law 5:15, 16
Hes 5:6, 7e Law 5:15
Law 7:1
Isa 53:10

f Law 5:18

g Kut 29:38-42
Hes 28:3
Ebr 10:11

Safu ya 2

a Kut 28:39
Law 16:32
Eze 44:17b Kut 28:42
Kut 39:27, 28c Kut 27:3
Law 1:16d Law 16:23
Eze 44:19

e Law 4:3, 12

f Law 1:7
Ne 13:30, 31

g Law 3:5, 16

h Law 2:1
Hes 15:3, 4i Law 2:2, 9
Law 5:11, 12j Law 2:3
Law 5:13
Eze 44:29
IKo 9:13

k Law 10:12

l Law 2:11

hani atavaa vazi lake rasmi la kitani^a na suruali fupi ya kitani.^{*b} Kisha ataondoa majivu^{#c} ya dhabihu iliyoteketezwa kwenye madhabahu na kuyaweka kando ya madhabahu. **11** Halafu atavua mavazi hayo^d na kuvaa mengine, naye atapeleka majivu hayo mahali safi nje ya kambi.^e **12** Ni lazima moto wa madhabahu uzendelee kuwaka. Haupaswi kuzimika. Kila asubuhi kuhani ataongeza kuni^f kwenye moto huo na kupanga dhabihu ya kuteketezwa juu yake, naye atateketeza mafuta ya dhabihu za ushirika ili yafuke moshi.^g **13** Hakikisheni kwamba moto unaendelea kuwaka daima kwenye madhabahu. Haupaswi kuzimika.

14 “‘Hii ndiyo sheria kuhusu toleo la nafaka:^h Ninyi wana wa Haruni mtamtolea Yehova toleo hilo mbele ya madhabahu. **15** Mmoja wenu atachukua mkono mmoja wa unga laini wa toleo la nafaka na kiasi fulani cha mafuta yake na ubani wote ulio katika toleo la nafaka, naye atauteketeza ili ufuke moshi kwenye madhabahu kama harufu ya kupendeza^{*} ya dhabihu ya kumbukumbu[#] kwa Yehova.ⁱ **16** Haruni na wanawe watatumia unga unaobaki kuoka mikate isiyo na chachu, nao watakula mikate hiyo mahali patakatifu. Wataila katika ua wa hema la mkutano.^k **17** Haipaswi kuokwa pamoja na kitu chochote chenye chachu.^l Nimewapa liwe

6:10 *Au “suruali ya ndani.” #Au “majivu yenye mafuta,” yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhabihu. **6:15** *Au “inayotuliza.” #Au “ukiwa sehemu ya ukumbusho (uwakilishi) wake.”

fungu lao kutoka katika matoleo yangu yanayochomwa kwa moto.^a Ni toleo takatifu kabisa,^b kama ilivyo dhabihu ya dhambi na dhabihu ya hatia. **18** Kila mzao wa kiume wa Haruni ataila.^c Ni posho yao ya kudumu katika vizazi vyenu vyote kutoka kwa matoleo ya Yehova yanayochomwa kwa moto.^d Chochote kinachogusa matoleo hayo kitakuwa kitakatifu.”

19 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **20** “Hivi ndivyo vitu ambavyo Haruni na wanawe watamtolea Yehova siku ambayo Haruni atatiwa mafuta:^e sehemu ya kumi ya kipimo cha efa moja^{*f} ya unga laini kama toleo la kawaida la nafaka,^g nusu ya unga huo asubuhi na nusu nyengine jioni. **21** Utachanganywa na mafuta na kuokwa kwenye kiokeo.^h Mtaukanda vizuri kabisa kwa mafuta na kuuleta ukiwa vitumbua vya toleo la nafaka lenye harufu inayompendeza* Yehova. **22** Mwana wa Haruni atakayetiwa mafuta ili kuwa kuhani baada yakeⁱ atatoa toleo hilo. Ni sheria ya kudumu: Kwa kuwa toleo hilo linatolewa kwa Yehova likiwa zima litateketezwa ili moshi ufuke mbele zake. **23** Kila toleo la nafaka la kuhani linapaswa kuwa toleo zima. Halipaswi kuliwa.”

24 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **25** “Mwambie hivi Haruni na wanawe: ‘Hii ndiyo sheria kuhusu dhabihu ya dhambi:^j Mnyama wa

6:20 *Sehemu ya kumi ya efa ilikuwa sawa na lita 2.2 au kilogramu 1.3 hivi. Angalia Nyongeza B14. **6:21** *Au “inayomtuliza.”

SURA YA 6

a Hes 18:9

b Law 2:3, 10

c Hes 18:10

d Law 24:8, 9

e Kut 30:30
Ebr 5:1

f Kut 16:36

g Kut 29:1, 2
Kut 29:40, 41
Law 2:1
Law 9:17
Hes 28:4, 5h Law 2:5
Law 7:9
1Nya 23:29

i Kum 10:6

j Law 4:3

Safu ya 2

a Law 1:3, 11

b Law 10:17
Hes 18:9
Eze 44:29c Kut 27:9
Law 6:14, 16
Eze 42:13d Law 6:14, 18
Law 21:21, 22
Hes 18:10

e Law 6:25

f Law 4:5
Law 10:18
Law 16:27
Ebr 13:11

SURA YA 7

g Law 5:6
Law 6:6
Law 14:2, 12
Law 19:20, 21
Hes 6:12

h Ebr 9:22

i Law 3:1, 2
Law 5:9j Kut 29:13, 14
Law 3:9, 17
Law 4:8, 9
Law 8:18, 20

k Law 3:3, 4

dhabihu ya dhambi atachinjiswa^a mahali ambapo mnyama wa dhabihu ya kuteketezwa huchinjwa mbele za Yehova. Ni dhabihu takatifu kabisa. **26** Kuhani anayetoa dhabihu hiyo kwa ajili ya dhambi ataila.^b Ataila mahali patakati-fu katika ua wa hema la mku-tano.^c

27 “Kila kitu kinachogusa nyama hiyo kitakuwa kitakatifu, na vazi la mtu yeyote likidondokewa na damu ya mnyama huyo, mtalifua vazi hilo mahali patakati-fu.

28 Chombo cha udongo kilichotumiwa kuchemshia nyama hiyo kitavunjwawunjwa. Lakini ikiwa ilichemshiwa katika chombo cha shaba, basi lazima chombo hicho kisuguliwe na kusafishwa kwa maji.

29 “Kila mwanamume kuhani ataila.^d Ni takatifu kabisa.^e **30** Lakini kila dhabihu ya dhambi ambayo kiasi fulani cha damu yake kimele-twa mahali patakati-fu kwenye hema la mkutano ili kufunika dhambi, haitaliwa.^f Itateketezwa.

7 “Hii ndiyo sheria kuhusu dhabihu ya hatia:^g Ni dhabihu takatifu kabisa. **2** Mnyama wa dhabihu ya hatia atachinjwa mahali ambapo dhabihu za kuteketezwa huchinjwa, na damu yake^h itanyunyizwa pande zote za madhabahu.ⁱ **3** Kuhani atatoa mafuta yote^j ya mnyama huyo pamoja na mkia wake wenye mafuta, mafuta yanayofunika matumbo, **4** na figo zake mbili pamoja na mafuta yake yaliyo karibu na kiuno. Ataondoa pia figo pamoja na mafuta yaliyo juu ya ini.^k

5 Kuhani ataviteketeza vitu

hivyo kwenye madhabahu ili vifuke moshi vikiwa dhahibu kwa Yehova inayochoywa kwa moto.^a Ni dhahibu ya hatia. **6** Kila mwanamume kuhani ataila,^b nayo inapaswa kuliwa mahali patakatifu. Ni dhahibu takatifu kabisa.^c **7** Sheria kuhusu dhahibu ya dhambi ni sawa na sheria kuhusu dhahibu ya hatia; dhahibu hiyo ni ya kuhani aliyeitoa kufunika dhambi.^d

8 “Kuhani akitoa dhahibu ya kuteketewa kwa ajili ya mtu, ngozi^e ya mnyama aliyeletwa kwa ajili ya dhahibu ya kuteketewa itakuwa ya kuhani huyo.

9 “Kila toleo la nafaka linalookwa kwenye jiko au kikaangio au kiokeo^f ni la kuhani anayelitwa. Litakuwa lake.^g **10** Lakini kila toleo la nafaka linalochanganywa na mafuta^h au lililo kavuⁱ litakuwa la wana wote wa Haruni; kila mmoja wao atapokea kiasi kilekile.

11 “Sasa hii ndio sheria ya dhahibu ya ushirika^j ambayo mtu yeyote anaweza kumtolea Yehova: **12** Ikiwa anaitoa ili kuonyesha shukrani,^k ataitoa dhahibu hiyo ya shukrani pamoja na mikate ya mviringo isiyo na chachu na iliyokandwa kwa mafuta, mikate myembamba isiyo na chachu na ambayo imepakwa mafuta, na mikate ya mviringo iliyookwa kwa unga laini uliochanganywa vizuri kabisa na kukandwa kwa mafuta. **13** Ataitoa dhahibu yake pamoja na mikate ya mviringo iliyotiwa chachu na dhahibu ya shukrani ya dhahibu zake za ushirika. **14** Ataitoa mkate mmoja kutoka katika kila toleo kuwa

SURA YA 7

a Law 3:14-16

b Law 5:13
Law 6:14, 16
Hes 18:9

c Law 2:3

d Law 6:25, 26
Law 14:13e Kut 29:14
Law 1:6f Law 6:20, 21
1Nya 23:29g Law 2:3-7
Hes 18:9
1Ko 9:13

h Law 14:21

i Law 5:11
Hes 5:15j Law 3:1
Law 7:20
Law 22:21
1Ko 10:16k Law 22:29
2Nya 29:31

Safu ya 2

a Law 6:25, 26
Law 10:14
Hes 18:8

b Law 22:29, 30

c Law 22:21

d Law 22:23
Kum 12:5, 6

e Law 19:5, 6

f Law 19:7, 8

g Hes 19:20

h Law 12:2, 4

i Law 11:21-24
Kum 14:7j Law 11:10
Kum 14:10k Law 3:16, 17
Law 4:8-10
1Sa 2:16, 17

fungu takatifu kwa Yehova; litakuwa la kuhani anayenyunyiza damu ya dhahibu za ushirika.^a **15** Nyama za dhahibu za ushirika zinazotolewa ili kuonyesha shukrani zinapaswa kuliwa siku ambayo dhahibu hiyo ya shukrani inatolewa. Nyama yoyote ya dhahibu hiyo haipaswi kuachwa mpaka asubuhi.^b

16 “Ikiwa dhahibu anayotoa ni kwa ajili ya nadhiri^c au ni toleo la hiari,^d inapaswa kuliwa siku ambayo anatoa dhahibu hiyo, na nyama inayobaki inaweza pia kuliwa siku inayofuata. **17** Lakini nyama yoyote inayobaki ya dhahibu hiyo inapaswa kuteketezwa siku ya tatu.^e **18** Hata hivyo, nyama yoyote ya dhahibu ya ushirika ikiliwa siku ya tatu, yule anayeitoa hatapata kibali. Haitamnufaisha; ni dhahibu inayochukiza, na mtu anayeila ataadhibiwa kwa sababu ya kosa lake.^f **19** Nyama inayogusa kitu chochote kisicho safi haipaswi kuliwa. Itateketezwa kwa moto. Mtu yeyote aliye safi anaweza kula nyama iliyo safi.

20 “Lakini mtu yeyote asiye safi akila nyama ya dhahibu ya ushirika, ambayo ni ya Yehova, ni lazima auawe.^g **21** Mtu yeyote akigusa kitu chochote kisicho safi, iwe ni uchafu wa mwanadamu^h au mnyama asiye safiⁱ au kitu chochote chenye kuchukiza kisicho safi,^j kisha ale nyama ya dhahibu ya ushirika, ambayo ni ya Yehova, ni lazima auawe.”

22 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **23** “Waaambia Waisraeli, ‘Hampaswi kula mafuta yoyote^k ya ng’o-

mbe dume au ya mwana-kondoo dume au ya mbuzi. **24** Mafuta ya mnyama ali-yepatikana amekufa na mafuta ya mnyama aliyeuawa na mnyama mwingine, yanaweza kutumiwa kwa kusudi lingine lolote, lakini hampaswi kamwe kuyala.^a **25** Kwa maana mtu yeyote anayekula mafuta ya mnyama anayemtoa kuwa dhabihu kwa Yehova inayochomwa kwa moto, ni lazima auawe.

26 “Hampaswi kula damu yoyote^b mahali popote mnapoishi, iwe ni damu ya ndege au ya mnyama. **27** Mtu yeyote anayekula damu ni lazima auawe.”^c

28 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **29** “Waabie Waisraeli, ‘Mtu yeyote anayemlelea Yehova dhabihu yake ya ushirika atamotolea Yehova sehemu ya dhabihu hiyo.^d **30** Ataleta mafuta^e pamoja na kidari kwa mikonu yake mwenyewe ili vitu hivyo viwe dhabihu kwa Yehova inayochomwa kwa moto, naye atavitikisa kwenda mbele na nyuma vikiwa toleo la kutikiswa^f mbele za Yehova. **31** Kuhani atayateketeza mafuta hayo kwenye madhabihu ili yafuke moshi,^g lakini kidari kitakuwa cha Haruni na wanawe.^h

32 “Mtampa kuhani mguu wa kulia kutoka katika dhabihu zenu za ushirika ukilwa fungu takatifu.ⁱ **33** Mguu wa kulia utakuwa fungu la mwana wa Haruni atakayetoa damu ya dhabihu za ushirika na mafuta.^j **34** Kwa maana nachukua kidari cha toleo la kutikiswa na mguu wa lile fungu takatifu kutoka kwa

SURA YA 7

a Kut 22:31
Law 17:15

b Mwa 9:4
Law 3:17
Law 17:10
Kum 12:16
1Sa 14:33
Mdo 15:20, 29

c Law 17:14

d Law 3:1

e Law 3:3

f Kut 29:24
Law 8:25-27
Law 9:21

g Law 3:3-5

h Law 8:29

i Kut 29:27, 28
Law 10:14
Hes 6:20

j Kum 18:3

Safu ya 2

a Law 10:14

b Kut 28:1
Kut 29:4, 7
Kut 40:13

c Kut 40:15
Law 8:12

d Law 6:9

e Law 2:1
Law 6:14

f Law 6:25

g Law 5:6
Law 7:1

h Kut 29:1
Law 6:20

i Law 3:1

j Kut 34:27

k Law 1:2

SURA YA 8

l Kut 28:1

m Kut 28:4
Kut 39:33, 41

n Kut 30:23-25
Kut 40:15

o Kut 29:1, 2

dhabihu za ushirika za Waisraeli na kumpa kuhani Haruni na wanawe. Ni sheria ya kudumu kwa Waisraeli.^a

35 “Hilo ndilo fungu lililotengwa kwa ajili ya makuhani, yaani, Haruni na wanawe, kutoka katika dhabihu za Yehova zinazochomwa kwa moto, fungu lililotengwa kwa ajili yao siku waliyowekwa rasmi kumtumikia Yehova wakiwa makuhani.^b **36** Yehova aliwaamuru Waisraeli wawape makuhani fungu hilo siku alipowatia mafuta.^c Ni sheria ya kudumu katika vizazi vyao.”

37 Hizo ndizo sheria kuhusu dhabihu ya kuteketezwa,^d toleo la nafaka,^e dhabihu ya dhambi,^f dhabihu ya hatia,^g dhabihu ya kuwaweka rasmi makuhani,^h na dhabihu ya ushirika,ⁱ **38** kama Yehova alivyomwamuru Musa kwenye Mlima Sinai^j siku aliyo waamuru Waisraeli wamtolea Yehova dhabihu zao katika nyika ya Sinai.^k

8 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Mchukue Haruni na wanawe,^l pamoja na mavazi yao,^m na mafuta yanayotumiwa kutia mafuta,ⁿ ng’ombe dume wa dhabihu ya dhambi, kondoo dume wawili, na kikapu cha mikate isiyo na chachu,^o **3** uwakusanye Waisraeli wote kwenye mlango wa hema la mkutano.”

4 Basi Musa akafanya kama Yehova alivyomwamuru, Waisraeli wote wakakusanyika kwenye mlango wa hema la mkutano. **5** Musa akawambia: “Hili ndilo jambo ambalo Yehova ameamuru tufanye.”

6 Kwa hiyo Musa akamleta Haruni na wanawe na kuwaosha kwa maji.^a **7** Kisha akamvisha kanzu,^b akamfunga ukumbuu,^c akamvisha lile joho lisilo na mikono,^d akamvisha efodi^e na kumfunga vizuri kabisa mshipi wa efodi uliofumwa.^f **8** Halafu akamvisha kifuko cha kifuani^g na kutia Urimu na Thumimu^h ndani ya kifuko hicho. **9** Kisha akamvisha kilembaⁱ kichwani na kuweka lile bamba linalong'aa la dhahabu upande wa mbele wa kilemba hicho, ile ishara takatifu ya wakfu,^{*j} kama Yehova alivyomwamuru Musa.

10 Kisha Musa akachukua mafuta yanayotumiwa kutia mafuta akalitia mafuta hema la ibada na vitu vyote vilivyokuwa ndani yake,^k akavitakasa. **11** Baada ya hayo akanyunyiza kiasi fulani cha mafuta hayo juu ya madhabahu mara saba na kuitia mafuta madhabahu, vyombo vyake vyote, na pia beseni na kinara chake, ili kuvitakasa. **12** Mwishowe akamimina juu ya kichwa cha Haruni kiasi fulani cha mafuta hayo yanayotumiwa kutia mafuta, akamtia mafuta ili kumtakasa.^l

13 Halafu Musa akawaleta wana wa Haruni, akawavisha kanzu, akawafunga ukumbuu, na kuwavisha kofia,^m kama Yehova alivyomwamuru Musa.

14 Kisha akamleta ng'ombe dume wa dhabihu ya dhambi, Haruni na wanawe wakaweka mikono yao juu ya kichwa cha ng'ombe dume huyo wa dhabihu ya dhambi.ⁿ **15** Musa akamchinja, aka-

SURA YA 8

a Kut 29:4
Kut 40:12

b Kut 28:39

c Kut 39:27, 29

d Kut 39:22

e Kut 28:6
Kut 39:2

f Kut 28:8
Kut 29:5
Kut 39:20

g Kut 28:15
Kut 39:9

h Kut 28:30

i Kut 29:6
Kut 39:27, 28

j Kut 28:36
Kut 39:30

k Kut 30:26-28

l Kut 29:4, 7
Kut 30:30
Kut 40:13
Law 21:10
Zb 133:2

m Kut 28:40
Kut 29:8, 9

n Kut 29:10-14
Law 4:3, 4
Law 16:6

Safu ya 2

a Ebr 9:21, 22

b Law 4:8, 9

c Law 4:11, 12
Law 16:27

d Kut 29:15-18
Law 1:4

e Law 8:33

chukua damu yake^a kwa kidole chake na kuzipaka pembe zote za madhabahu, akaitakasa madhabahu kutokana na dhambi, lakini damu iliyobaki aliimwaga kwenye msingi wa madhabahu, ili aitakase na kutoa juu yake dhabihu ya kufunika dhambi. **16** Kisha Musa akachukua mafuta yote yaliyofunika matumbo, mafuta yaliyo juu ya ini, na figo mbili pamoja na mafuta yake, akateketeza vitu hivyo juu ya madhabahu ili vifuke moshi.^b **17** Kisha akachukua sehemu zilizobaki za ng'ombe dume huyo, ngozi yake, nyama yake, na mavi yake, akateketeza sehemu hizo nje ya kambi,^c kama Yehova alivyomwamuru Musa.

18 Halafu akamleta kondoo dume wa dhabihu ya kuteketezwa, Haruni na wanawe wakaweka mikono yao juu ya kichwa cha kondoo dume huyo.^d

19 Musa akamchinja na kunyunyiza damu yake pande zote za madhabahu. **20** Akamkata kondoo huyo vipande vipande, akateketeza kichwa, vipande alivyokata, na mafuta yaliyo kwenye figo, ili vifuke moshi. **21** Akaosha matumbo na miguu kwa maji na kumtekeza kondoo dume mzima kwenye madhabahu ili afuke moshi. Ilikuwa dhabihu ya kuteketezwa yenye harufu inayopendeza.^{*} Ilikuwa dhabihu kwa Yehova inayochomwa kwa moto, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

22 Kisha akamleta kondoo dume wa pili, kondoo wa kuwaweka rasmi makuhani,^e basi Haruni na wanawe wa-

8:9 *Au "lile taji takatifu."

8:21 *Au "inayotuliza."

kaweka mikono yao juu ya kichwa cha kondoo huyo.^a **23** Musa akamchinja na kuchukua kiasi fulani cha damu yake na kuipaka kwenye ncha ya sikio la kulia la Haruni na kwenye kidole gumba cha mkono wake wa kulia na kwenye kidole gumba cha mguu wake wa kulia. **24** Kisha Musa akawaleta wana wa Haruni na kuwapaka damu hiyo kwenye ncha za masikio yao ya kulia na kwenye vidole gumba vya mikono yao ya kulia na kwenye vidole gumba vya miguu yao ya kulia; lakini damu iliyobaki Musa aliinyunyiza pande zote za madhabahu.^b

25 Kisha akachukua yale mafuta, mkia wenye mafuta, mafuta yote yaliyofunika matumbo, mafuta yote yaliyokuwa juu ya ini, zile figo mbili na mafuta yake, na mguu wa kulia.^c **26** Akachukua mkate mmoja wa mvingingo usio na chachu,^d mkate mmoja wa mvingingo wenye mafuta,^e na mkate mmoja mwembamba kutoka katika kikapu cha mikate isiyo na chachu kilichokuwa mbele za Yehova. Akaiweka mikate hiyo juu ya vipande vya mafuta na juu ya mguu wa kulia. **27** Baada ya hayo akaviweka vitu hivyo vyote katika mikono ya Haruni na mikono ya wanawe na kuanza kuvitikisa kwenda mbele na nyuma wikiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova. **28** Kisha Musa akavichukua kutoka mikononi mwao na kuviteketeza kwenye madhabahu juu ya dhabihu ya kuteketezwa ili vifuke moshi. Vitu hivyo vilikuwa dhabihu ya kuwaweka rasmi makuha-

SURA YA 8

a Kut 29:19, 20

b Kut 24:6

c Kut 29:22-25

d Law 2:4

e Kut 29:1, 2

Safu ya 2

a Law 7:29, 30

b Kut 29:26, 27
Law 7:34, 35

c Kut 30:30

d Hes 3:2, 3

e Kut 29:21

f Law 6:28

g Kut 29:31, 32
1Ko 9:13

h Kut 29:34

i Kut 29:30, 35
Hes 3:2, 3j Kut 29:36
Law 17:11

k Kut 29:37

ni, dhabihu yenye harufu ya kupendeza.* Vilikuwa dhabihu kwa Yehova inayochomwa kwa moto.

29 Kisha Musa akachukua kidari na kukitikisa kwenda mbele na nyuma kikiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova.^a Sehemu hiyo ya kondoo wa kuwaweka rasmi makuhani ilikuwa fungu la Musa, kama Yehova alivyomwamuru Musa.^b

30 Halafu Musa akachukua kiasi kidogo cha mafuta yanayotumiwa kutia mafuta^c na kiasi kidogo cha damu iliyokuwa kwenye madhabahu, akamnyunyizia Haruni na mavazi yake na pia wanawe na mavazi yao. Basi akamtakasa Haruni na mavazi yake na pia wanawe^d na mavazi yao.^e

31 Kisha Musa akamwambia Haruni na wanawe: "Chemsheni^f nyama hiyo kwenye mlango wa hema la mkutano, na muile hapo mlangoni pamoja na mikate iliyo katika kikapu cha kuwaweka rasmi makuhani, kama nilivyoamriwa kwamba, 'Haruni na wanawe wataila.'^g **32** Mtateketeza nyama na mikate itakayobaki.^h **33** Hampaswi kutoka nje ya mlango wa hema la mkutano kwa siku saba, mpaika siku zenu za kuwekwa rasmi kuwa makuhani zitakapokwisha, kwa sababu itachukua muda wa siku saba kuwaweka rasmi kuwa makuhani.ⁱ **34** Yehova alituumuru tufanye mambo tuliyoanya leo ili tuwatolee dhabihu ya kufunika dhambi zenu.^j **35** Mtakaa kwenye mlango wa hema la mkutano kwa siku saba,^k

8:28 * Au "kutuliza."

mchana na usiku, nanyi mta-timiza wajibu wenu mbele za Yehova,^a msije mkafa; hivyo ndivyo nilivyoamriwa.”

36 Basi Haruni na wanawe wakafanya mambo yote ambayo Yehova aliamuru kupitia Musa.

9 Siku ya nane,^b Musa akamwita Haruni na wanawe na wazee wa Israeli. **2** Akamwambia Haruni: “Chukua ndama mchanga kwa ajili ya dhabihu ya dhambi^c na kondoo dume kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa, wanyama wasio na kasoro, nawe uwatoe mbele za Yehova. **3** Lakini utawaambia Waisraeli ‘Chukueni mbuzi dume kwa ajili ya dhabihu ya dhambi na ndama na mwanakondoo dume, wote wa umri wa mwaka mmoja na wasio na kasoro, kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa, **4** na ng’ombe dume na kondoo dume kwa ajili ya dhabihu za ushirika,^d ili muwatoe dhabihu mbele za Yehova, na pia toleo la nafaka^e lililochanganywa na mafuta, kwa sababu leo Yehova atawatokea.”^f

5 Basi wakapeleka vitu ambavyo Musa aliamuru mbele ya hema la mkutano. Halafu Waisraeli wote wakaja na kusimama mbele za Yehova.

6 Musa akasema: “Hili ndilo jambo ambalo Yehova amewaamuru mfanye, ili muone utukufu wa Yehova.”^g **7** Kisha Musa akamwambia Haruni: “Nenda kwenye madhabahu, utoe dhabihu yako ya dhambi^h na dhabihu yako ya kuteketezwa, utoe dhabihu ya kufunika dhambi zako mwenyeweⁱ na za nyumba yako; ki-

SURA YA 8

a Hes 1:53

SURA YA 9

b Law 8:35

c Law 4:3

d Law 3:1

e Law 2:4
Law 6:14

f Kut 29:43

g Kut 16:10
Kut 24:16
Kut 40:34

h Law 4:3

i Ebr 7:27

Safu ya 2

a Law 16:33
Ebr 5:1-3

b Law 4:3, 4

c Ebr 9:22

d Law 4:7
Law 8:14, 15

e Law 4:8-10

f Law 4:11, 12
Ebr 13:11

g Law 1:5

h Law 1:3
Law 6:9

i Law 2:1, 11, 13

sha uwatolee watu dhabihu ya kufunika dhambi zao,^a kama Yehova alivyoamuru.”

8 Haruni akaenda mara moja kwenye madhabahu na kumchinja yule ndama za dhabihu ya dhambi kwa ajili yake mwenyewe.^b **9** Kisha wanawe wakamletea damu,^c naye akachovya kidole chake katika damu hiyo na kupaka pembe za madhabahu, na damu iliyobaki akaimwaga kwenye msingi wa madhabahu.^d **10** Akateketeza mafuta na figo na mafuta yaliyo juu ya ini kutoka katika dhabihu ya dhambi ili vifuke moshi kwenye madhabahu, kama Yehova alivyomwamuru Musa.^e **11** Naye akateketeza nyama na ngozi nje ya kambi.^f

12 Kisha Haruni akamchinja mnyama wa dhabihu ya kuteketezwa na wanawe wakampa damu, naye akainyunyiza pande zote za madhabahu.^g **13** Wakampa vipande vya mnyama wa dhabihu ya kuteketezwa pamoja na kichwa, naye akaviteketeza ili vifuke moshi kwenye madhabahu. **14** Pia, akao-sha matumbo na miguu, akaviteketeza vitu hivyo kwenye madhabahu juu ya dhabihu ya kuteketezwa ili vifuke moshi.

15 Kisha akatoa dhabihu kwa ajili ya watu; akamchukua yule mbuzi wa dhabihu ya dhambi aliyepaswa kutolewa kwa ajili ya watu, akamchinja na kutoa dhabihu ya dhambi kama alivyofanya kwa yule wa kwanza. **16** Akatoa dhabihu ya kuteketezwa akifuata utaratibu wa kawaida.^h

17 Kisha akatoa toleo la nafaka;ⁱ akachukua mkono mmo-

ja wa toleo hilo na kuliteketeza ili lifuke moshi kwenye madhabahu pamoja na dhabihu ya kuteketezwa ya asubuhi.^a

18 Baada ya hayo Haruni akamchinja yule ng'ombe dume na kondoo dume wa dhabihu ya ushirika aliye-paswa kutolewa kwa ajili ya watu. Kisha wanawe wakampa damu, akainyunyiza pande zote za madhabahu.^b **19** Lakini vipande vyenye mafuta vya ng'ombe dume,^c mkia we-nyye mafuta wa kondoo dume, mafuta yaliyofunika matumbo, na figo, na mafuta yaliyokuwa juu ya ini,^d **20** waliwiweka vipande hivyo vyote vyenye mafuta juu ya vidari, kisha akaviteketeza vipande hivyo ili vifuke moshi kwenye madhabahu.^e **21** Hata hivyo, Haruni akatikisa vidari na mguu wa kulia kwenda mbele na nyuma kuwa toleo la kutikisa mbele za Yehova, kama Musa alivyoamuru.^f

22 Kisha Haruni akainua mikono yake kuelekea watu, akawabariki,^g naye akashuka chini baada ya kutoa dhabihu ya dhambi na dhabihu ya kuteketezwa na dhabihu za ushirika. **23** Mwishowe Musa na Haruni wakaingia katika hema la mkutano, kisha wakatoka nje na kuwabariki watu.^h

Ndipo watu wote wakaona utukufu wa Yehova,ⁱ **24** na moto ukashuka kutoka kwa Yehova^j na kuanza kuteketeza ile dhabihu ya kuteketezwa na vile vipande vyenye mafuta vilivyokuwa kwenye madhabahu. Watu wote walipoo-na hilo, wakaanza kupaza sauti na kuanguka kifudufudi.^k

SURA YA 9

a Kut 29:39

b Law 3:1, 2

c Law 3:3, 4

d Law 3:9, 10

e Law 7:29-31

f Kut 29:27, 28

g Hes 6:23-27
Kum 10:8
Kum 21:5
1Nya 23:13h 2Sa 6:18
2Nya 6:3

i Law 9:6

j Amu 6:21
1Nya 21:26k 1Fa 18:38, 39
2Nya 7:1, 3

Safu ya 2

SURA YA 10

a Kut 6:23
1Nya 24:2b Kut 30:34, 35
Law 16:12c Kut 30:9
Law 10:9
Law 16:1, 2

d Hes 16:35

e Hes 26:61

f Kut 19:22

g Kut 6:18

h Law 21:10

i Kut 28:41
Law 8:12
Law 21:11, 11, 12

j Eze 44:21

MAMBO YA WALAWI 9:18-10:9

10 Baadaye Nadabu na Abihu,^a wana wa Haruni, walichukua kila mmoja wao chetezo chake, wakaweka moto ndani yake na kutia uvumba.^b Wakaanza kumtolea Yehova moto haramu,^c jambo ambalo hakuwaamuru wafanye. **2** Ndipo moto ukashuka kutoka kwa Yehova, ukawateketeza,^d wakafa mbele za Yehova.^e **3** Musa akamwambia Haruni: "Yehova amesema hivi: 'Nitatakaswa miongoni mwa wale walio karibu nami,^f nami nitatukuzwa mbele ya watu wote.'" Haruni akanyamaza kimya.

4 Basi Musa akamwita Mishaeli na Elsafani, wana wa Uzieli,^g ndugu ya baba ya Haruni, akawaambia: "Njooi hapa, waondoeni ndugu zenu mbele ya mahali patakatifu muwapeleke nje ya kambi."

5 Kwa hiyo wakaja, wakawabeba wakiwa na kanzu zao na kuwapeleka nje ya kambi, kama Musa alivyowaambia.

6 Kisha Musa akamwambia Haruni na wanawe waliobaki, Eleazari na Ithamari: "Msikose kutunza nywele zenu na msirarue mavazi yenu,^h msije mkafa na kumfanya Mungu awakasirikie Waisraeli wote. Ndugu zenu wote wa nyumba ya Israeli watawaombolezea wale ambao Yehova amewaan-gamiza kwa moto. **7** Msitoke nje ya mlango wa hema la mkutano msije mkafa, kwa sababu Yehova amewatia mafuta."ⁱ Basi wakafanya kama Musa alivyosema.

8 Kisha Yehova akamwambia Haruni: **9** "Wewe na wanao msinywe divai au kileo chochote mnapoingia katika hema la mkutano,^j msije

mkafa. Ni sheria ya kudumu katika vizazi vyenu. **10** Ili muweze kutofautisha mambo matakatiifu na mambo yaliyo najisi, mambo safi na mambo yasiyo safi,^a **11** na ili muwafundishe Waisraeli wote sheria zote ambazo* Yehova ameambia kupitia Musa.”^b

12 Kisha Musa akamwambia Haruni na wanawe waliobaki, Eleazari na Ithamari: “Chukueni toleo la nafaka lililobaki kutoka katika dhambi-hu za Yehova zinazochomwa kwa moto, mle toleo hilo karibu na madhabahu kama mkate usio na chachu,^c kwa sababu ni toleo takatifu kabisa.^d **13** Mtakula toleo hilo mahali patakatifu,^e kwa sababu ni posho yenu na posho ya wana wenu kutoka kwenye dhambi-hu za Yehova zinazochomwa kwa moto, kwa maana hivyo ndivyo nilivyoamriwa. **14** Pia, wewe na wanao na binti zako^f mtakula kidari cha toleo la kutikiswa na mguu wa fungu takatifu^g mkiwa mahali safi kwa sababu vitu hivyo vimetolewa ili kuwa posho yako na posho ya wanao kutoka kwenye dhambi-hu za ushirika za Waisraeli. **15** Watauleta mguu wa fungu takatifu na kidari cha toleo la kutikiswa pamoja na dhambi-hu za mafuta zinazochomwa kwa moto, ili vitikiswe mbele za Yehova vikiwa toleo la kutikiswa kwenda mbele na nyuma; hilo litakuwa posho yako na posho ya kudumu ya wanao,^h kama Yehova alivyoamuru.”

16 Musa akamtafuta sana mbuzi wa dhambi-hu ya dhambi,ⁱ lakini akagundua kwamba alikuwa ameteketezwa. Kwa hiyo

10:11 * Au “masharti yote ambayo.”

SURA YA 10

a Eze 44:23

b Kum 33:10
2Nya 17:8, 9
Ne 8:7, 8
Mal 2:7

c Law 6:14, 16

d Law 21:22

e Law 6:26
Hes 18:10

f Law 22:13
Hes 18:11

g Kut 29:26-28
Law 7:31, 34
Law 9:21

h 1Ko 9:13

i Law 9:3, 15

Safu ya 2

a Law 6:25, 26
Eze 44:29

b Law 6:29, 30

c Law 9:8, 12

SURA YA 11

d Kum 14:4-6
Eze 4:14

e Kum 14:7, 8

f Met 30:26

g Isa 65:4
Isa 66:3, 17

akawakasirikia sana Eleazari na Ithamari, wana walio-baki wa Haruni, akawauliza: **17** “Kwa nini hamkula dhambi-hu ya dhambi mkiwa mahali patakatifu,^a wakati ni dhambi-hu takatifu kabisa ambayo amewapa ili mbebe dhambi za Waisraeli wote na kuwatolea dhambi-hu ya kufunika dhambi zao mbele za Yehova? **18** Sasa angalieni! Damu yake haijale-twa mahali patakatifu.^b Mlipaswa kula dhambi-hu hiyo mahali patakatifu, kama nilivyoamriwa.” **19** Haruni akamjibu Musa: “Tazama! Leo walimtolea Yehova dhambi-hu yao ya dhambi na dhambi-hu yao ya kuteketezwa,^c na bado mambo haya yamenipata. Kama ninge-kula dhambi-hu ya dhambi leo, je, jambo hilo lingempe-ndeza Yehova?” **20** Musa aliposikia hayo, akaridhika.

11 Kisha Yehova akawaa-ambia Musa na Haruni: **2** “Waambieni Waisraeli, ‘Hawa ndio wanyama wa nchi kavu mnaoweza kula.’^d **3** Mnaweza kumla kila mnyama mwenye kwato zilizopasuka na zilizogawanyika anayecheua.

4 “Lakini hampaswi kuwala wanyama wafuatao wanaocheua au wenye kwato zilizogawanyika: msimle ngamia kwa sababu anacheua lakini kwato zake hazijagawanyika. Yeye si safi kwenu.^e **5** Pia, msimle wibarif kwa sababu anacheua lakini kwato zake hazijagawanyika. Yeye si safi kwenu. **6** Pia, msimle sungura kwa sababu anacheua lakini kwato zake hazijagawanyika. Yeye si safi kwenu. **7** Pia, msimle nguruwe^g kwa sababu ana kwato zilizopa-

suka na kugawanyika lakini hacheui. Yeye si safi kwenu. **8** Msile kamwe nyama yao wala kugusa mizoga yao. Hao si safi kwenu.^a

9 “Kati ya viumbe wote wanaoishi ndani ya maji, mna-weza kula wafuatao: Mna-weza kumla kiumbe yeyote wa majini mwenye mapezi na magamba anayeishi baharini au mtoni.^b **10** Lakini kiumbe yeyote anayeishi baharini na mtoni ambaye hana mapezi na magamba, kati ya viumbe wote wa majini wanaoishi katika makundi makubwa na viumbe wengine wote wanaoishi majini, ni chukizo kwenu. **11** Naam, watakuwa chukizo kwenu, msile kamwe nyama yao,^c nanyi mnapaswa kuchukua mizoga yao. **12** Kiumbe yeyote wa majini ambaye hana mapezi na magamba ni chukizo kwenu.

13 “Hawa ndio ndege mnapaswa kuchukua; wasiliwe kwa sababu ni chukizo: tai,^d furukombe, tumbusi* mweusi,^e **14** mwewe mwekundu na aina zote za mwewe weusi, **15** kila aina ya kunguru, **16** mbuni, bundi, shakwe, kila aina ya kipanga, **17** bundi mdogo, mnandi, bundi mwenye masikio marefu, **18** batamaji, mwari, tumbusi,* **19** korongo, kila aina ya kulastara, hudihudi, na popo. **20** Kila kiumbe mwenye mabawa* anayeishi katika makundi makubwa anayetambaa kwa miguu yote minne ni chukizo kwenu.

21 “Kati ya wadudu wote wenye mabawa wanaoishi katika makundi makubwa na wa-

11:13, 18 *Au “tai mla mizoga.” 11:20 *Au “kila mdudu.”

SURA YA 11

a Mdo 10:14

b Kum 14:9, 10

c Kum 14:3

d Ayu 39:27, 30

e Kum 14:12-19

Safu ya 2

a Mt 3:4
Mk 1:6

b Law 14:46, 47
Law 15:8
Law 17:15
Law 22:4-6

c Law 14:2, 8
Law 15:2, 5
Hes 19:10

d Kum 14:7, 8

e Law 17:15, 16

f Law 5:2

g Isa 66:17

h Kum 14:19

i Law 11:24
Law 22:4, 5

naotambaa kwa miguu yote minne, mna-weza kula tu wadudu wenye vifundo miguuni wanaoruka ardhini. **22** Hawa ndio mnaoweza kula: kila aina ya nzige wanaohama, nzige wengine wanaoliwa,^a chenene,* na panzi. **23** Wadudu wengine wote wenye mabawa wanaoishi katika makundi makubwa wenye miguu minne ni chukizo kwenu. **24** Wadudu hao watawafanya msiwe safi. Kila mtu anayegusa mizoga yao hatakuwa safi mpaka jioni.^b **25** Kila mtu anayebeba mizoga yao anapaswa kufua mavazi yake;^c hatakuwa safi mpaka jioni.

26 “Mnyama yeyote mwenye kwato zilizopasuka lakini hazijagawanyika na ambaye hacheui si safi kwenu. Kila mtu anayewagusa wanyama hao hatakuwa safi.^d **27** Kila kiumbe anayetembea kwa miguu yenye makucha kati ya viumbe wanaotembea kwa miguu minne si safi kwenu. Kila mtu anayegusa mizoga yao hatakuwa safi mpaka jioni. **28** Yeyote atakayebeba mizoga yao anapaswa kufua mavazi yake,^e hatakuwa safi mpaka jioni.^f Hao si safi kwenu.

29 “Hawa ndio viumbe wanaotambaa ambao si safi kwenu: fuko, panya,^g kila aina ya mjusi, **30** mjusi kafiri, mju-si mkubwa, mjusi wa majini, mjusi wa mchangani, na kinyonga. **31** Viumbe hao wanaotambaa si safi kwenu.^h Kila mtu anayegusa mizoga yao hatakuwa safi mpaka jioni.ⁱ

32 “Viumbe hao wakifa na kuangukia kitu chochote, kitu hicho hakitakuwa safi, iwe ni

11:22 *Au “nyenje.”

chombo cha mbao, nguo, ngozi, au gunia. Chombo chocho-
te kinachotumiwa kinapaswa
kutumbukizwa majini, nacho
hakitakuwa safi mpaka jioni;
baada ya hapo kitakuwa safi.
33 Wakianguka ndani
ya chombo cha udongo, mna-
paswa kukivunja, na chocho-
te kilichokuwa ndani ya cho-
mbo hicho si safi.^a **34** Cha-
kula chochote kinachomwa-
gikiwa na maji kutoka katika
chombo hicho si safi, na ki-
nywaji chochote kutoka kati-
ka chombo hicho si safi.
35 Kitu chochote kinachoa-
ngukiwa na mizoga yao si safi.
Vitu hivyo vitavunjwavyunja
iwe ni jiko kubwa au dogo.
Vitu hivyo si safi, navyo havi-
takuwa safi kwenu. **36** Hata
hivyo, chemchemi au tan-
gi la maji litabaki safi, laki-
ni mtu yeyote anayegusa mi-
zoga yao hatakuwa safi.
37 Mizoga yao ikiangukia
mbegu za kupandwa, zitabaki
safi. **38** Lakini mbegu zikiti-
wa maji kisha sehemu yoyote
ya mizoga yao iangukie mbe-
gu hizo, mbegu hizo si safi
kwenu.

39 “Mnyama yeyote mna-
yeruhusiwa kula akifa, yeyote
anayegusa mzoga wake
hatakuwa safi mpaka jioni.^b
40 Yeyote anayekula sehemu
yoyote ya mzoga huo anapa-
swa kufua mavazi yake, ha-
takuwa safi mpaka jioni.^c Na
yeyote anayebeba mzoga huo
anapaswa kufua mavazi yake,
naye hatakuwa safi mpaka jio-
ni. **41** Kila kiumbe anayeta-
mbaa ni chukizo.^d Hapaswi
kuliwa. **42** Hampaswi kumla
kiumbe yeyote anayetambaa
kwa tumbo, kiumbe yeyote
anayetembea kwa miguu yote

SURA YA 11

a Law 15:12

b Law 11:23, 24
Hes 19:11, 16c Law 17:15
Law 22:3, 8
Kum 14:21
Eze 4:14
Eze 44:31

d Law 11:21

Safu ya 2

a Kum 14:3

b Law 20:25

c Kut 20:2

d Kut 19:6
Law 19:2
Kum 14:2
1Th 4:7e 1Pe 1:15, 16
Ufu 4:8f Kut 6:7
Kut 29:46
Ho 11:1g Kut 22:31
Hes 15:40
Kum 7:6h Law 20:7, 26
Yos 24:19
1Sa 2:2i Law 20:25
Eze 44:23

SURA YA 12

j Law 15:19

k Mwa 17:12
Mwa 21:4
Lu 1:59
Lu 2:21, 22
Yoh 7:22

minne, au viumbe wowote wa-
naoishi katika makundi maku-
bwa wenye miguu mingi, kwa
sababu viumbe hao ni chuki-
zo.^a **43** Msinifanye niwachu-
kie kwa kula kiumbe yeyote
kati ya viumbe hao, msijitie
unajisi na kuwa watu wasio
safi.^b **44** Kwa maana mimi ni
Yehova Mungu wenu,^c nanyi
lazima mjitakase na kuwa wa-
takatifu,^d kwa sababu mimi
ni mtakatifu.^e Kwa hiyo msi-
jichafue kwa kula kiumbe ye-
yote anayetambaa. **45** Kwa
maana mimi ni Yehova, nina-
yewaongoza kupanda kutoka
nchini Misri ili nijithibiti-
she mwenyewe kuwa Mungu
wenu,^f nanyi lazima muwe wa-
takatifu,^g kwa sababu mimi ni
mtakatifu.^h

46 “Hiyo ndiyo sheria ku-
husu wanyama, ndege, kila
kiumbe anayeishi majini,
na kila kiumbe anayetambaa,
47 ili kutofautisha viumbe
walio safi na wasio safi na
viumbe wanaoweza kuliwa na
wasioweza kuliwa.”ⁱ

12 Yehova akaendelea ku-
mwambia Musa: **2** “Wa-
ambie Waisraeli, ‘Mwanamke
akipata mimba na kuzaa mto-
to wa kiumbe, mwanamke huyo
hatakuwa safi kwa siku saba,
atakuwa kama anavyokuwa
katika siku zake za hedhi.’
3 Siku ya nane, mtoto huyo
atahiriwa.^k **4** Kisha kwa
siku 33 mwanamke huyo atae-
ndelea kujitakasa kwa saba-
bu ya damu aliyopoteza. Asi-
guse kitu chochote kitakatifu,
wala asiingie mahali pataka-
tifu mpaka atakapokamilisha
siku zake za kujitakasa.

5 “Akizaa mtoto wa kike,
mwanamke huyo hatakuwa
safi kwa siku 14, atakuwa

kama anavyokuwa katika siku zake za hedhi. Kisha atae-ndelea kujitakasa kwa siku 66 kwa sababu ya damu aliyopoteza. **6** Siku zake za kujitakasa zitakapokwisha baada ya kuzaa mtoto wa kiume au wa kike, atamletea kuhani mwanakondoo dume wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa^a na hua mchanga au njiwa tetere kwa ajili ya dhabihu ya dhambi kwenye mlango wa hema la mkutano. **7** Kuhani atatoa dhabihu hizo mbele za Yehova ili kufunika dhambi ya mwanamke huyo, kisha atakuwa safi kutokana na damu yake. Hiyo ndiyo sheria kuhusu mwanamke anayezaa mtoto wa kiume au wa kike. **8** Lakini ikiwa hawezi kuleta kondoo, basi anapaswa kuleta njiwa tetere wawili au hua wawili wachanga,^b mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa na wa pili kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, naye kuhani atamtolea dhabihu hizo ili kufunika dhambi yake, kisha atakuwa safi.”

13 Yehova akaendelea kuwaambia Musa na Haruni: **2** “Ikiwa mtu ana uvimbe kwenye ngozi yake, au upele, au kigaga, au doa ambalo linaweza kuwa ugonjwa wa ukoma,^{*c} anapaswa kupeleka kwa kuhani Haruni au kwa mmoja wa wanawe, makuhani.^d **3** Kuhani atachunguza sehemu iliyoathiriwa ya ngozi. Ikiwa nywele za se-

13:2 *Neno la Kiebrania linalotafsiriwa “ukoma” lina maana pana na linaweza kutia ndani magonjwa mbalimbali ya ngozi yanayoambukiza. Linaweza pia kutia ndani maambukizi fulani yaliyopatikana kwenye nguo na nyumba.

SURA YA 12

a Law 1:10

b Law 1:14
Law 5:7
Law 14:21, 22
Lu 2:24

SURA YA 13

c Hes 12:10, 12
2Nya 26:19
Mt 8:3d Kum 24:8
Eze 44:23
Mal 2:7
Lu 17:14

Safu ya 2

a Law 13:50
Law 14:38
Hes 12:15b Mt 8:4
Mk 1:44
Lu 5:14
Lu 17:14c Law 13:15, 25,
30, 42
Hes 12:10, 12

d Law 13:3

e Law 13:24, 25

hemu hiyo zimebadilika kuwa nyeupe na ugonjwa umepenya chini ya ngozi, huo ni ugonjwa wa ukoma. Kuhani ataachunguza na kutangaza kwamba mtu huyo si safi. **4** Lakini ikiwa ana doa jeupe kwenye ngozi na inaonekana halijapenya chini ya ngozi na nywele hazijabadilika kuwa nyeupe, basi kuhani atamtenga mtu huyo kwa siku saba.^a **5** Kisha kuhani atamchunguza siku ya saba, na ugonjwa huo ukioonekana kwamba hauendelei, nao haujaenea kwenye ngozi, atamtenga kwa siku nyingine saba.

6 “Kuhani anapaswa kuchunguza tena siku ya saba, na ikiwa ugonjwa huo umefiia na haujaenea katika ngozi, kuhani atatangaza kwamba mtu huyo ni safi;^b kilikuwa kigaga tu. Kisha mtu huyo atafua mavazi yake na kuwa safi. **7** Lakini ikiwa ni wazi kwamba kigaga hicho kimeenea* kwenye ngozi baada ya mtu huyo kwenda kwa kuhani kuthibitisha utakaso wake, basi atafika tena[#] mbele ya kuhani. **8** Kuhani atachunguza kigaga hicho, na ikiwa kimeenea kwenye ngozi, atatangaza kwamba mtu huyo si safi. Huo ni ukoma.^c

9 “Mtu akishikwa na ukoma, ni lazima apelekwe kwa kuhani, **10** kisha kuhani atamchunguza.^d Ikiwa ana uvimbe mweupe kwenye ngozi na nywele za sehemu hiyo zimebadilika kuwa nyeupe na uvimbe huo umebadilika kuwa kidonda kibichi,^e **11** huo ni ukoma wa muda mrefu,

13:7 *Au “ambukizo hilo limeenea.”
[#]Au “mara ya pili.”

kuhani atatangaza kwamba mtu huyo si safi. Hapaswi kumtenga,*^a kwa kuwa si safi.

12 Lakini ikiwa ukoma umeenea kwenye ngozi yote na kufunika mwili mzima kuanzia kichwani mpaka miguuni, kwa kadiri ambayo kuhani anaona, **13** na kuhani amemchunguza na kuona kwamba ukoma umefunika ngozi yake yote, atatangaza kwamba mtu huyo ni safi.* Ngozi yote imekuwa nyeupe, yeye ni safi.

14 Lakini akipata kidonda kibichi, hatakuwa safi. **15** Kuhani akikiona kidonda hicho kibichi, atatangaza kwamba mtu huyo si safi.^b Kidonda hicho kibichi si safi. Ni ukoma.^c

16 Lakini kidonda hicho kikiabadilika tena na kuwa cheupe, mtu huyo ataenda kwa kuhani. **17** Kuhani atamchunguza,^d na ikiwa kimebadilika kuwa cheupe, kuhani atamtangaza kuwa safi mtu huyo aliyeambukizwa.

18 "Mtu akishikwa na jipu kisha lipone, **19** na uvimbe mweupe au doa lenye mchanganyiko wa rangi nyekundu na nyeupe litokee mahali palipokuwa na jipu hilo, ni lazima aende kwa kuhani. **20** Kuhani atachunguza doa hilo,^e na akiona kwamba limepenya chini ya ngozi na nywele za sehemu hiyo zimebadilika kuwa nyeupe, atatangaza kwamba mtu huyo si safi. Ni ugonjwa wa ukoma uliotokea mahali palipokuwa na jipu. **21** Lakini kuhani akichunguza na kuona kwamba hakuna nywele nyeupe sehemu hiyo na doa halijapenya chini

13:11 *Yaani, hapaswi kumtenga kwa uchunguzi zaidi. 13:13 *Au "hawezi kuwaambukiza wengine."

SURA YA 13

a Law 13:4

b Kum 24:8

c Law 13:8

d Lu 5:14
Lu 17:14

e Eze 44:23

Safu ya 2

a Law 13:4, 50
Law 14:38
Hes 12:15

b Mt 8:4
Mk 1:44
Lu 5:14
Lu 17:14

c Law 13:4, 50
Law 14:38
Hes 12:15

d Kum 24:8
Mal 2:7

ya ngozi, nalo limeanza kupona, atamtenga kwa siku saba.^a

22 Na ikiwa limeenea kwenye ngozi, kuhani atatangaza kwamba mtu huyo si safi. Ni ugonjwa. **23** Lakini doa hilo likibaki palepale na halijaenea, ni uvimbe tu wa jipu, kuhani atamtangaza kuwa safi.^b

24 "Au ikiwa mtu ana kovu lililosababishwa na moto na kovu hilo bichi likigeuka rangi na kuwa doa lenye mchanganyiko wa rangi nyekundu na nyeupe au nyeupe tu, **25** kuhani atalichunguza doa hilo. Ikiwa nywele zimebadilika na kuwa nyeupe katika doa hilo na inaonekana limepenya chini ya ngozi, ni ukoma uliotokea kwenye kovu, basi kuhani atatangaza kwamba mtu huyo si safi. Ni ugonjwa wa ukoma.

26 Lakini kuhani akichunguza doa hilo na kuona halina nywele nyeupe, halijapenya chini ya ngozi, na limeanza kupona, atamtenga mtu huyo kwa siku saba.^c **27** Kuhani atamchunguza siku ya saba, na ikiwa limeenea kwenye ngozi, atatangaza kwamba mtu huyo si safi. Ni ugonjwa wa ukoma. **28** Lakini doa hilo likibaki vilevile na lisipoenea kwenye ngozi, na ikiwa limeanza kupona, ni uvimbe tu wa lile kovu, kuhani atatangaza kwamba mtu huyo ni safi, kwa sababu ni mwasho wa kovu hilo.

29 "Mwanamume au mwanamke akipata kidonda kichwani au kwenye kidevu, **30** kuhani atachunguza kidonda hicho.^d Akiona kwamba kimepenya chini ya ngozi na nywele za sehemu hiyo ni za manjano na ni chache, kuhani atatangaza kwamba mtu huyo

si safi; ni ugonjwa unaoathiri ngozi ya kichwa au kidevu. Ni ukoma wa kichwa au wa kidevu. **31** Lakini kuhani akiona kwamba kidonda hicho hakijapenya chini ya ngozi na sehemu hiyo haina nywele nyeusi, anapaswa kumtenga mtu huyo kwa siku saba.^a **32** Kuhani atachunguza kidonda hicho siku ya saba, ikiwa hakijaenea au hakina nywele za manjano na hakijapenya chini ya ngozi, **33** mtu huyo anapaswa kunyolewa, lakini hata nyolewa sehemu yenye kidonda. Kisha kuhani atamtenga mtu huyo kwa siku saba.

34 "Kuhani atakichunguza tena kidonda hicho siku ya saba, na ikiwa kidonda hicho kilicho kichwani na kwenye kidevu hakijaenea au kupenya chini ya ngozi, kuhani anapaswa kutangaza kwamba mtu huyo ni safi, atafua mavazi yake na kuwa safi. **35** Lakini ikiwa kidonda kimeenea kwenye ngozi baada ya mtu huyo kutangazwa kuwa safi, **36** kuhani atamchunguza, ikiwa kidonda hicho kimeenea kwenye ngozi, kuhani ahitaji kuchunguza ikiwa kuna nywele za manjano; mtu huyo si safi. **37** Lakini akimchunguza na kuona kwamba hakijaenea na nywele nyeusi zimeota sehemu iliyokuwa na kidonda, mtu huyo amepona. Yeye ni safi, kuhani atamtangaza kuwa safi.^b

38 "Mwanamume au mwanamke akiwa na madoa meupe kwenye ngozi, **39** kuhani atayachunguza.^c Ikiwa madoa hayo si meupe sana, ni vipele visivyo na madhara vilivyotokea kwenye ngozi. Mtu huyo ni safi.

SURA YA 13

a Law 13:4, 50
Law 14:38
Hes 12:15

b Mt 8:4
Mk 1:44
Lu 5:14
Lu 17:14

c Law 13:2

Safu ya 2

a Hes 5:2
Hes 12:14
2Fa 7:3
2Nya 26:20, 21

40 "Ikiwa mwanamume atapata upara kichwani, yeye ni safi. **41** Akipata upara sehemu ya mbele ya kichwa, yeye ni safi. **42** Lakini mtu akipata kidonda chenye mchanganyiko wa rangi nyekundu na nyeupe kwenye upara au paji la uso, ni ukoma unaotokea kwenye upara au paji lake la uso. **43** Kuhani atamchunguza, na ikiwa kidonda kilicho kwenye upara au paji lake la uso kina uvimbe wenywe mchanganyiko wa rangi nyekundu na nyeupe, na ngozi yake inaonekana ni kama ina ukoma, **44** mtu huyo ana ukoma. Yeye si safi, kuhani anapaswa kutangaza kwamba mtu huyo si safi kwa sababu ya ugonjwa aliopata kichwani. **45** Mtu mwenye ukoma anapaswa kuvaa mavazi yaliyoraruka, hapaswi kutunza nywele za kichwa chake, naye anapaswa kufunika masharubu yake na kusema hivi kwa sauti: 'Mimi si safi, mimi si safi!' **46** Kwa muda wote atakaokuwa na ugonjwa huo hatakuwa safi. Kwa kuwa yeye si safi, ataishi akiwa ametengwa. Ataishi nje ya kambi.^a

47 "Vazi likiathiriwa na ugonjwa wa ukoma, iwe ni vazi la safu au la kitani, **48** iwe ni ndani ya mtande au ndani ya mshindio wa kitani au wa sufu, au ndani ya ngozi au ndani ya chochote kilichotengenezwa kwa ngozi, **49** na ikiwa vazi, ngozi, mtande, mshindio, au kitu chochote cha ngozi kina doa lenye mchanganyiko wa rangi ya manjano na kijani au doa jekundu, huo ni ugonjwa wa ukoma, kuhani anapaswa kuonyesha vazi hilo.

50 Kuhani atachunguza ugonjwa huo, naye anapaswa kulitenga vazi hilo lenye ugonjwa kwa siku saba.^a **51** Atakapolichunguza siku ya saba na kuona kwamba ugonjwa huo umeenea ndani ya vazi, ndani ya mtande, ndani ya mshindio, au ndani ya ngozi (haidhuru ngozi hiyo inatumiwa kwa kusudi gani), huo ni ukoma hatari, vazi hilo si safi.^b **52** Anapaswa kuliteketeza vazi hilo au mtande au mshindio wa sufu au wa kitani au kitu chochote cha ngozi kilichoathiriwa na ugonjwa huo, kwa sababu huo ni ukoma hatari. Ugonjwa huo unapaswa kutekelezwa.

53 “Lakini kuhani akichunguza na kuona kwamba ugonjwa haujaenea ndani ya vazi au ndani ya mtande au ndani ya mshindio au ndani ya kitu chochote cha ngozi, **54** ataamuru kitu kilichoathiriwa kioskwe, naye atakitenga kwa siku saba zaidi. **55** Baada ya kitu hicho kuoshwa kabisa, kuhani atakikagua. Ikiwa doa hilo halijabadilika, hata ikiwa ugonjwa haujaenea, kitu hicho si safi. Mnapaswa kukiteketeza kwa sababu kimeliwa na ukoma, iwe kime-liwa chini au ndani.

56 “Baada ya kitu hicho kuoshwa kabisa, kuhani atakikagua na akiona kwamba doa hilo limefifia, atararua sehemu iliyoathiriwa ya vazi au ngozi au mtande au mshindio. **57** Hata hivyo, doa hilo likitokea sehemu nyingine ya vazi au ndani ya mtande au ndani ya mshindio au ndani ya kitu chochote cha ngozi, ugonjwa huo unaenea, nanyi mnapaswa kutekeleza kitu chocho-

SURA YA 13

a Law 13:4
Law 14:38
Hes 12:15

b Law 14:44, 45

Safu ya 2

a Law 13:52

SURA YA 14

b Law 13:2

Mt 8:4
Mk 1:44
Lu 5:14
Lu 17:14

c Law 14:49-53
Hes 19:6, 9
Zb 51:7

d Law 16:22

te kilichoathiriwa.^a **58** Lakini ikiwa vazi au mtande au mshindio au kitu chochote cha ngozi hakina doa baada ya kuoshwa, kitu hicho kinapaswa kuoshwa mara ya pili, nacho kitakuwa safi.

59 “Hiyo ndiyo sheria kuhusu ugonjwa wa ukoma ulioathiri vazi la sufu au la kitani, au mtande au mshindio, au kitu chochote cha ngozi; itatumiwa kutangaza vitu hivyo kuwa safi au si safi.”

14 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Hii ndiyo sheria inayomhusu mtu mwenye ukoma ambayo inapaswa kufuatwa siku ambayo utakaso wake unathibitishwa, anapopelekwa kwa kuhani.^b

3 Kuhani atatoka nje ya kambi na kumchunguza. Ikiwa mtu mwenye ukoma amepona, **4** kuhani atamwamuru alete ndege safi wawili walio hai, tawi la mwerezi, kitambaa cha rangi nyekundu, na tawi la hisopo ili atakaswe.^c **5** Kuhani ataamuru ndege mmoja achinjwe kwenye chombo cha udongo chenye maji ya kijito.

6 Lakini anapaswa kumchukua ndege aliye hai na kumtumbukiza pamoja na tawi la mwerezi, kitambaa cha rangi nyekundu, na tawi la hisopo ndani ya damu ya ndege aliyechinjiwa kwenye maji ya kijito. **7** Kisha kuhani atachukua damu hiyo na kumnyunyizia mara saba mtu anayejitakasa ukoma wake na kumtangaza kuwa safi, halafu atamwachilia ndege aliye hai aende zake mashambani.^d

8 “Ni lazima mtu anayejitakasa afue mavazi yake, anyoe nywele zake zote, na kuoga kwa maji, kisha atakuwa safi.

Baada ya hayo, anaweza kurudi kambini, lakini atakaa nje ya hema lake kwa siku saba. **9** Siku ya saba anapaswa kunyoa nywele zote kichwani, ndevu zote, na kope zake. Baada ya kunyoa nywele zote, atafua mavazi yake na kuoga kwa maji, kisha atakuwa safi.

10 "Siku ya nane, ataleta wanakondoo dume wawili wasio na kasoro, mwanakondoo jike wa mwaka mmoja asiye na kasoro,^a na sehemu tatu za kumi za kipimo cha efa* ya unga laini uliochanganywa na mafuta kuwa toleo la nafaka,^b na logi moja[#] ya mafuta;^c **11** na kuhani anayemtangaza kuwa safi atamleta mtu huyo anayejitakasa na matoleo hayo mbele za Yehova kwenye mlango wa hema la mkutano. **12** Kuhani huyo atamchukua yule mwanakondoo dume na kumtoa kuwa dhambi ya hatia^d pamoja na ile logi moja ya mafuta, naye atavitikisa kwenda mbele na nyuma vikiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova.^e **13** Kisha atamchinja mwanakondoo huyo mahali ambapo dhambi za dhambi na dhambihu za kuteketezwa huchinjwa,^f mahali patakatifu, kwa sababu, sawa na dhambihu ya dhambi, dhambihu ya hatia ni ya kuhani.^g Ni dhambihu takatifu kabisa.^h

14 "Kisha kuhani atachukua kiasi kidogo cha damu ya dhambihu ya hatia na kupaka ncha ya sikio la kulia la mtu anayejitakasa na kidole gumba cha mkono wake

14:10 *Sehemu tatu za kumi za efa zili-kuwa sawa na lita 6.6 au kilogramu 3.9 hivi. Angalia Nyongeza B14. [#]Logi ili-kuwa sawa na lita 0.3. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 14

a Law 4:32

b Law 2:1

c Mk 1:44

d Law 6:6

e Law 14:21, 24

f Law 1:10, 11
Law 4:3, 4

g Law 2:3
Law 7:7
1Ko 9:13
1Ko 10:18

h Law 6:25

Safu ya 2

a Law 14:10

b Law 6:7
1Yo 1:7
1Yo 2:1, 2

c Law 5:6

d Law 2:1
Law 14:10
Hes 15:4

e Mt 8:4

f Law 14:9
Mk 1:44
Lu 5:14
Lu 17:14

wa kulia na kidole gumba cha mguu wake wa kulia. **15** Halafu kuhani atachukua kiasi kidogo cha ile logi ya mafuta^a na kumimina kwenye kiganja chake mwenyewe cha mkonno wa kushoto. **16** Kisha kuhani atachovya kidole chake cha kulia katika mafuta yaliyo kwenye kiganja chake cha kushoto, atanyunyiza mara saba kwa kidole chake kiasi kidogo cha mafuta hayo mbele za Yehova. **17** Kisha kuhani atatia kiasi kidogo cha mafuta yaliyobaki kwenye kiganja chake na kupaka ncha ya sikio la kulia la mtu anayejitakasa na kidole gumba cha mkonno wake wa kulia na kidole gumba cha mguu wake wa kulia juu ya damu ya dhambihu ya hatia. **18** Kuhani atatia mafuta yaliyobaki kwenye kiganja chake na kumpaka kichwani mtu anayejitakasa, naye kuhani atamtotea mtu huyo dhambihu ya kufunika dhambi yake mbele za Yehova.^b

19 "Kuhani atatoa dhambihu ya dhambi^c na kumtolea dhambihu ya kufunika dhambi mtu anayejitakasa uchafu wake, kisha atamchinja mnyama wa dhambihu ya kuteketezwa. **20** Kuhani atatoa dhambihu ya kuteketezwa na toleo la nafaka^d kwenye madhabahu, naye atamtotea mtu huyo dhambihu ya kufunika dhambi yake,^e naye atakuwa safi.^f

21 "Hata hivyo, ikiwa mtu huyo ni maskini na hawezi kupata vitu hivyo, basi ataleta mwanakondoo dume mmoja atolewe kuwa dhambihu ya hatia na toleo la kutikiswa, ili atoe dhambihu ya kufunika dhambi yake, pia ataleta sehemu ya kumi ya kipimo cha

efa moja* ya unga laini uliochanganywa na mafuta ili uwe toleo la nafaka, logi ya mafuta, **22** na njiwa tetere wawili au hua wawili wachanga, kulingana na uwezo wake. Ndege mmoja atatolewa kuwa dhahihu ya dhambi na wa pili dhahihu ya kuteketezwa.^a **23** Siku ya nane^b atawaleta kwa kuhani kwenye mlango wa hema la mkutano mbele za Yehova ili kuthibitisha utakaso wake.^c

24 "Kuhani atamchukua mwanakondoo dume wa dhahihu ya hatia^d na logi ya mafuta na kuvitikisa kwenda mbele na nyuma vikiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova.^e **25** Kisha atamchinja kondoo dume mchanga wa dhahihu ya hatia na kuchukua kiasi kidogo cha damu ya dhahihu ya hatia na kupaka ncha ya sikio la kulia la mtu anayejitakasa na kidole gumba cha mkono wake wa kulia na kidole gumba cha mguu wake wa kulia.^f **26** Kuhani atamimina kiasi kidogo cha mafuta hayo kwenye kiganja chake mwenyewe cha mkono wa kushoto,^g **27** kisha atanyuniza kwa kidole chake cha kulia kiasi kidogo cha mafuta yaliyo kwenye kiganja chake cha kushoto mara saba mbele za Yehova. **28** Naye atatia kiasi kidogo cha mafuta yaliyo kwenye kiganja chake na kupaka ncha ya sikio la kulia la mtu anayejitakasa na kidole gumba cha mkono wake wa kulia na kidole gumba cha mguu wake wa kulia sehemu zilezile alizompaka damu ya dhahihu ya hatia. **29** Kisha kuhani

14:21 *Sehemu ya kumi ya efa ilikuwa sawa na lita 2.2 au kilogramu 1.3 hivi. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 14

a Law 1:14
Law 5:7
Law 12:8

b Law 15:13,14

c Law 14:10,11

d Law 6:6

e Law 14:12

f Law 14:14

g Law 14:15-18

Safu ya 2

a Law 12:8
Law 14:22

b Law 5:7

c Law 14:20

d Hes 35:10

e Mwa 17:8

f Kum 7:12,15

atatia mafuta yaliyobaki kwenye kiganja chake na kumpaka kichwani mtu anayejitakasa ili amtolee mtu huyo dhahihu ya kufunika dhambi yake mbele za Yehova.

30 "Atatoa njiwa tetere mmoja kati ya wale wawili au hua mmoja mchanga kati ya wale wawili, kulingana na uwezo wake.^a **31** atatoa ndege anaoweza kupata, mmoja kwa ajili ya dhahihu ya dhambi na mwingine kwa ajili ya dhahihu ya kuteketezwa,^b ataleta pia toleo la nafaka; na kuhani atamtolea mtu huyo anayejitakasa dhahihu ya kufunika dhambi yake mbele za Yehova.^c

32 "Hiyo ndiyo sheria inayomhusu mtu aliyekuwa na ugonjwa wa ukoma lakini hana uwezo wakati wa kuthibitisha utakaso wake."

33 Kisha Yehova akamwambia Musa na Haruni:

34 "Mtakapoingia katika nchi ya Kanaani,^d ambayo ninawapa ili mwimiliki,^e nami niipige kwa ukoma nyumba fulani katika nchi yenu,^f **35** mwenye nyumba hiyo anapaswa kwenenda kwa kuhani na kumwambia, 'Nimeona madoa fulani ndani ya nyumba yangu.' **36** Kuhani ataagiza vitu vyote vilivyvo ndani ya nyumba hiyo vitolewe nje kabla hajaja kuikagua, ili asitangaze kwamba kila kitu kilicho katika nyumba hiyo si safi; baada ya hilo ataingia ndani na kuikagua. **37** Atachunguza sehemu zilizoathiriwa, na ikiwa kuta za nyumba hiyo zina sehemu zilizobonyea zenye mchanganyiko wa rangi ya manjano na kijani au rangi nyekundu, na sehemu hizo zinaonekana zimebonyea

sana ukutani, **38** basi kuhani atatoka nje ya mlango wa nyumba hiyo na kuifunga kwa siku saba.^a

39 “Kisha kuhani atarudi siku ya saba na kuikagua. Ikiwa madoa yameenea katika kuta za nyumba hiyo, **40** ndipo kuhani ataagiza mawe yaliyoathiriwa yabomolewe na kutupwa nje ya jiji, mahali pasipo safi. **41** Kisha ataagiza nyumba hiyo ikwanguliwe kabisa sehemu ya ndani, na lipu na saruji iliyondolewa itatupwa nje ya jiji, mahali pasipo safi. **42** Kisha wataleta mawe mengine na kuyaweka mahali ambapo mawe ya kwanza yalikuwepo; anapaswa kutumia saruji nyingine kuipiga lipu nyumba hiyo.

43 “Hata hivyo, madoa yakitokea tena na kuenea ndani ya nyumba hiyo baada ya mawe kubomolewa na nyumba kukwanguliwa na kupigwa lipu tena, **44** kuhani ataingia ndani na kuikagua. Ikiwa madoa hayo yameenea, nyumba hiyo ina ukoma hatari.^b Si safi. **45** Ataagiza nyumba hiyo ibomolewe, yaani, mawe yake, mbaao zake, na lipu yote katika nyumba hiyo, kisha vitu hivyo vitatupwa nje ya jiji, mahali pasipo safi.^c **46** Lakini mtu yeyote atakayeingia ndani ya nyumba hiyo siku yoyote itakapokuwa imetengwa,^d hatakuwa safi mpaka jioni;^e **47** na yeyote anayelala katika nyumba hiyo anapaswa kufua mavazi yake, na yeyote anayekula chakula katika nyumba hiyo anapaswa kufua mavazi yake.

48 “Hata hivyo, kuhani akija na kuona kwamba madoa

SURA YA 14

a Law 13:4, 50
Hes 12:15

b Law 13:51

c Law 14:41

d Law 14:38

e Law 11:23-25
Law 15:8
Law 17:15
Law 22:4-6

Safi ya 2

a Law 14:3, 4
Hes 19:6, 7

b Law 14:6, 7

c Law 13:30

d Law 13:47

e Law 14:34

f Law 13:2

g Law 10:10
Eze 44:23

h Kum 24:8

SURA YA 15

i Law 22:4
Hes 5:2

MAMBO YA WALAWI 14:38-15:2

hayajaenea baada ya nyumba hiyo kupigwa lipu tena, ataitangaza nyumba hiyo kuwa safi, kwa sababu ukoma umekwisha. **49** Ili kuitakasa nyumba hiyo isiyo safi,* atachukua ndege wawili, tawi la mwerezi, kitambaa cha rangi nyekundu, na tawi la hisopo.^a **50** Atamchinjia ndege mmoja kwenye chombo cha udongo chenye maji ya kijito. **51** Kisha atamchukua ndege aliye hai na kumtumbukiza pamoja na tawi la mwerezi, kitambaa cha rangi nyekundu, na tawi la hisopo ndani ya damu ya ndege aliyechinjwa kwenye maji ya kijito, naye atainyunyiza kuelekea nyumba hiyo mara saba.^b **52** Naye ataitakasa nyumba hiyo isiyo safi* kwa kutumia damu ya ndege huyo, maji ya kijito, yule ndege aliye hai, tawi la mwerezi, tawi la hisopo, na kitambaa cha rangi nyekundu. **53** Kisha atamwachilia ndege aliye hai aende zake mashambani nje ya jiji, naye ataitolea nyumba hiyo dhabihu ya kufunika dhambi, nayo itakuwa safi.

54 “Hiyo ndiyo sheria kuhusu aina mbalimbali za ukoma: ukoma wa kichwa au kidevu,^c **55** ukoma wa mavazi^d au nyumba,^e **56** uvimbe, vigaga, na madoa,^f **57** ili kuthibitisha ikiwa kitu ni safi au si safi.^g Hiyo ndiyo sheria kuhusu ukoma.”^h

15 Yehova akaendelea kuwaambia Musa na Haruni: **2** “Waambieni Waisraeli, ‘Mwanamume akitokwa na umajimaji kwenye kiungo chake cha uzazi,* umajimaji huo unamfanya asiwe safi.’ⁱ

14:49, 52 *Tnn., “yenyewe dhambi.” 15:2 *Tnn., “mwili wake.”

3 Yeye si safi kwa sababu ya umajimaji huo, iwe umajimaji huo unaendelea kutoka kati-ka kiungo chake cha uzazi au umezuwiwa kutoka, bado yeye si safi.

4 “Kitanda chochote anacholalia mtu anayetokwa na umajimaji hakitakuwa safi, na kitu chochote anachokalia hakitakuwa safi. **5** Mtu anayegusa kitanda cha mtu huyo ni lazima afue mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni.^a

6 Mtu yeyote anayeketi kwenye kitu kilichokaliwa na mtu anayetokwa na umajimaji anapaswa kufua mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni.

7 Mtu yeyote anayemgusa mtu anayetokwa na umajimaji anapaswa kufua mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni.

8 Mtu anayetokwa na umajimaji akimtemea mate mtu aliye safi, ni lazima mtu aliyetemewa mate ayafue mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni. **9** Matandiko yoyote yaliyo mgongoni mwa mnyama yatahayokaliwa na mtu anayetokwa na umajimaji hayatakuwa safi.

10 Mtu yeyote anayegusa kitu chochote kilichokaliwa na mtu huyo hatakuwa safi mpaka jioni, na yeyote anayebeba vitu hivyo atafua mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni. **11** Mtu anayetokwa na umajimaji^b akimgusa mtu mwingine bila kuna-wa mikono, ni lazima mtu aliyeguswa afue mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni.

12 Chombo cha udongo kinachoguswa na mtu anayetokwa na umajimaji kinapaswa kuvunjwa, na chombo chochote cha mbaao kinapaswa kusafishwa kwa maji.^a

13 “Mtu aliyekuwa akitokwa na umajimaji akipona na kuwa safi, atangoja kwa siku saba ili atakaswe, na ni lazima afue mavazi yake na kuoga kwenye maji wa kijito, naye atakuwa safi.^b **14** Siku ya nane, anapaswa kuchukua njiva tetere wawili au hua wawili wachanga^c na kwenda mbele za Yehova, kwenye mlango wa hema la mkutano na kumpa kuhani ndege hao. **15** Kisha kuhani atamtoa ndege mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi na ndege wa pili kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa, naye kuhani atamtotea mtu huyo dhabihu ya kufunika dhambi yake mbele za Yehova ili awe safi kutokana na umajimaji wake.

16 “Mwanamume akitokwa na shahawa, anapaswa kuoga mwili mzima kwenye maji naye hatakuwa safi mpaka jioni.^d **17** Ni lazima afue kwa maji vazi lolote na ngozi yoyote iliyomwagikiwa na shahawa, na vitu hivyo havitakuwa safi mpaka jioni.

18 “Mwanamume akilala na mwanamke kisha atokwe na shahawa, wote wawili wanapaswa kuoga kwenye maji na hawatakuwa safi mpaka jioni.^e

19 “Ikiwa mwanamke anatokwa na damu ya hedhi, hatakuwa safi kwa siku saba.^f Mtu yeyote anayemgusa hatakuwa safi mpaka jioni.^g

20 Kitu chochote anacholalia muda wote ambao yeye

SURA YA 15

a Law 11:24, 25
Law 14:46, 47
Law 17:15
Law 22:6

b Law 15:2

Safu ya 2

a Law 11:32, 33

b Law 14:8

c Law 1:14

d Law 22:4
Kum 23:10, 11

e Kut 19:15
1Sa 21:5

f Law 12:2, 5

g Law 20:18

fupi*^a ya kitani inapaswa kufunika mwili wake,[#] na anapaswa kujifunga ukumbuu wa kitani^b na kuvaa kilemba cha kitani^c kichwani. Ni mavazi matakatifu.^d Ataoga kwenye maji^e na kuyavaa.

5 "Anapaswa kuchukua kutoka kwa Waisraeli^f wanambuzi dume wawili kwa ajili ya dhabihu ya dhambi na kondoo dume mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa.

6 "Kisha Haruni atamtoa yule ng'ombe dume wa dhabihu ya dhambi kwa ajili yake mwenyewe, naye atatoa dhabihu ya kufunika dhambi zake mwenyewe^g na za nyumba yake.

7 "Halafu atachukua wale mbuzi wawili na kuwapeleka mbele za Yehova kwenye mlango wa hema la mkutano.

8 Haruni atapiga kura kwa ajili ya mbuzi hao wawili, kura moja ya Yehova na nyingine ya Azazeli.* 9 Haruni atamchukua yule mbuzi aliyechaguliwa kwa kura^h kuwa wa Yehova na kutoa dhabihu ya dhambi.

10 Lakini yule mbuzi aliyechaguliwa kwa kura kuwa wa Azazeli anapaswa kupeleka akiwa hai mbele za Yehova ili dhabihu ya kufunika dhambi itolewe juu yake, kusudi aachiliwe aende zake nyikani akiwa wa Azazeli.

11 "Haruni atamtoa yule ng'ombe dume wa dhabihu ya dhambi, ambaye anatolewa kwa ajili yake mwenyewe, na kutoa dhabihu ya kufunika dhambi zake mwenyewe na za nyumba yake; kisha ata-

SURA YA 16

a Kut 28:42

b Kut 39:27, 29

c Kut 28:4

d Kut 28:2

e Kut 30:20
Ebr 10:22

f Ebr 7:27

g Ebr 5:1-3

h Met 16:33

i Law 14:7, 53
Law 16:21, 22
Isa 53:4
Ro 15:3

Safu ya 2

a Law 16:6

b Ebr 9:4

c Kut 40:29
Law 6:13
Hes 16:46

d Kut 30:34-36
Ufu 5:8
Ufu 8:3-5

e Law 16:2
Ebr 6:19
Ebr 10:19, 20

f Kut 25:22
2Fa 19:15

g Kut 25:18, 21
1Nya 28:11

h Kut 34:29

i Ebr 9:22

j Ro 3:25
Ebr 9:12
Ebr 9:24, 25
Ebr 10:4, 12

k Law 16:5
Ebr 2:17
Ebr 5:1-3
Ebr 9:26
1Yo 2:1, 2

l Ebr 6:19
Ebr 9:3, 7
Ebr 10:19, 20

m Law 17:11

n Mhu 7:20

mchinja ng'ombe dume huyo wa dhabihu ya dhambi, anayetolewa kwa ajili yake mwenyewe.^a

12 "Halafu atachukua chezezo^b kilichojaa makaa ya moto kutoka katika madhabahu^c mbele za Yehova na mikono miwili iliyojaa uvumba bora uliotiwa manukato,^d naye ataleta vitu hivyo nyuma ya pazia.^e 13 Pia atatia uvumba huo juu ya moto mbele za Yehova,^f na moshi wa uvumba huo utafunika kifuniko cha sanduku la agano,^g kilicho juu ya ule Ushahidi,^h asije akafa.

14 "Atachukua kiasi fulani cha damu ya ng'ombe dumeⁱ na kuinyunyiza kwa kidole chake mbele ya kifuniko upande wa mashariki, atanyunyiza kiasi fulani cha damu hiyo mara saba mbele ya kifuniko hicho.^j

15 "Kisha atamchinja yule mbuzi wa dhabihu ya dhambi kwa ajili ya watu^k na kuleta damu yake nyuma ya pazia,^l atafanya kama alivyofanya na damu^m ya yule ng'ombe dume; atainyunyiza kuelekea hicho kifuniko na mbele ya hicho kifuniko.

16 "Ni lazima atoe dhabihu ya kufunika dhambi kwa ajili ya mahali patakatifu kwa sababu ya uchafu, makosa, na dhambi za Waisraeli,ⁿ na hivyo ndivyo anavyopaswa kufanya kwa ajili ya hema la mkutano ambalo liko miongoni mwao katikati ya uchafu wao.

17 "Hakuna mtu mwingine yeyote anayepaswa kuwa ndani ya hema la mkutano kuanzia wakati Haruni anapoiingia mahali patakatifu kutoa

16:4 *Au "suruali ya ndani." # Au "uchi wake." 16:8 *Huenda neno hili linamaanisha "Mbuzi Anayetoweka."

dhahihu ya kufunika dhambi, mpaka anapotoka nje. Atatoa dhahihu ya kufunika dhambi zake mwenyewe na za nyumba yake^a na za kusanyiko lote la Waisraeli.^b

18 “Kisha atatoka nje na kwenda kwenye madhabahu^c iliyo mbele za Yehova, naye atatoa dhahihu ya kufunika dhambi kwa ajili ya madhabahu hiyo, kisha atachukua kiasi fulani cha damu ya yule ng’ombe dume na kiasi fulani cha damu ya yule mbuzi na kupaka pembe za madhabahu pande zote. **19** Pia atainyunyiza madhabahu kiasi fulani cha damu hiyo mara saba kwa kidole chake na kuisafisha na kuitakasa kwa sababu ya uchafu wa Waisraeli.

20 “Baada ya kutoa dhahihu ya kufunika dhambi^d kwa ajili ya mahali patakatifu, hema la mkutano, na madhabahu,^e atamtoa pia yule mbuzi aliye hai.^f **21** Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha mbuzi huyo aliye hai na kuungama juu yake makosa yote ya Waisraeli na maovu yao yote na dhambi zao zote, ataziweka juu ya kichwa cha mbuzi^g huyo na kumwagiza mtu aliyechaguliwa* ampeleke mbuzi huyo nyikani. **22** Mbuzi huyo atazibeba dhambi zao zote^h na kuzipeleka jangwani,ⁱ mtu huyo atampeleka mbuzi huyo na kumwacha aende zake nyikani.^j

23 “Kisha Haruni ataingia katika hema la mkutano na kuyavua yale mavazi ya kitani aliyovaa alipoingia mahali patakatifu, naye atayaweka chini humo. **24** Ni lazima aoge

16:21 *Au “aliye tayari.”

SURA YA 16

a Law 16:6

b Mk 10:45
Ebr 2:9
Ebr 7:27
Ebr 9:7,12
Ufu 1:5

c Kut 38:1

d Ebr 9:23

e Law 16:16

f Law 16:8,10

g Isa 53:5,6
Zko 5:21h Isa 53:12
Efe 1:7
Ebr 9:28
1Pe 2:24
1Yo 3:5i Zb 103:12
Ebr 13:12

j Law 16:10

Safu ya 2

a Kut 30:20

b Kut 28:4
Law 8:7

c Law 16:3

d Law 16:5

e Efe 1:7

f Law 16:8,21

g Law 4:11,12
Ebr 13:11,12h Law 23:27,28
Hes 29:7i Yoh 3:16
Ro 8:32
Tit 2:13,14
1Yo 1:7
1Yo 3:16j Yer 33:8
Ebr 9:13,14
Ebr 10:2

k Law 23:32

mwili wake kwa maji^a mahali patakatifu na kuvaa mavazi yake;^b kisha atatoka nje na kutoa dhahihu yake ya kuteketezwa^c na dhahihu ya watu ya kuteketezwa;^d atatoa dhahihu ya kufunika dhambi zake mwenyewe na za watu wote.^e **25** Atayateketeza mafuta ya dhahihu ya dhambi ili yafuke moshi kwenye madhabahu.

26 “Yule mtu aliyempeleka mbuzi wa Azazeli^f anapaswa kufua mavazi yake na kuoga kwenye maji, kisha anaweza kurudi kambini.

27 “Yule ng’ombe dume wa dhahihu ya dhambi na yule mbuzi wa dhahihu ya dhambi, ambao damu yao ililetwa mahali patakatifu ili itumiwe kufunika dhambi, watapeleka nje ya kambi, na ngozi zao na nyama yao na mavi yao vitateketezwa motoni.^g **28** Mtu atakayeteketeza vitu hivyo anapaswa kufua mavazi yake na kuoga kwenye maji, kisha anaweza kurudi kambini.

29 “Ifuatayo itakuwa sheria ya kudumu kwa ajili yenu: Katika mwezi wa saba, siku ya kumi ya mwezi huo, mnapaswa kujitesa,* hampaswi kufanya kazi yoyote,^h awe ni mwenyeji au mgeni anayeishi miongoni mwenu. **30** Siku hiyo dhahihu ya kufunika dhambiⁱ itatolewa kwa ajili yenu ili mtangazwe kuwa safi. Mtasafishwa dhambi zenu zote mbele za Yehova.^j **31** Ni sabato ya pumziko kamili kwenu, mnapaswa kujitesa.*^k Ni sheria ya kudumu.

16:29 *Kwa ujumla inaeleweka kwamba “kujitesa” kunamaanisha kujinyima kwa njia mbalimbali, kutia ndani kufunga. 16:31 *Au “kuitesa nafsi yenu.”

32 “Kuhani atakayetiwa mafuta^a na kuwekwa rasmi*^b ili atumike akiwa kuhani baada ya baba yake,^c atatoa dhahibu ya kufunika dhambi na kuvaa yale mavazi matakatifu^d ya kitani.^e **33** Atatoa dhahibu ya kufunika dhambi kwa ajili ya mahali patakati-fu,^f hema la mkutano,^g na madhabahu;^h naye atatoa dhahibu ya kufunika dhambi za makuhani na za watu wote.ⁱ

34 Hiyo itakuwa sheria ya kudumu kwa ajili yenu^j ili dhahibu ya kufunika dhambi itolewe kwa ajili ya Waisraeli ili kufunika dhambi zao zote mara moja kila mwaka.”^k

Basi Haruni akafanya kama Yehova alivyomwamuru Musa.

17 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Mwambie Haruni na wanawe na Waisraeli wote, ‘Yehova amearuru hivi:

3 ““Mwisraeli yeyote aki-mchinja ng’ombe dume au mwanakondoo dume au mbuzi ndani au nje ya kambi, **4** na kukosa kumleta kwenye mlango wa hema la mkutano ili kumtolea Yehova dhahibu mbele ya hema la Yehova la ibada, mtu huyo atakuwa na hatia ya damu. Ameua,* naye ni lazima auawe. **5** Itakuwa hivyo ili Waisraeli wamletee Yehova dhahibu wanazotolea mashambani, wamletee kuhani dhahibu hizo kwenye mlango wa hema la mkutano. Wanapaswa kumtolea Yehova dhahibu hizo zikiwa dhahibu za ushirika.^l **6** Naye kuhani atainyunyizia madhabahu ya

16:32 *Tnn., “ambaye mkono wake utajazwa.” 17:4 *Tnn., “Amemwaga damu.”

SURA YA 16

a Kut 29:4, 7
Law 8:12

b Law 8:33

c Hes 20:26

d Kut 28:39
Kut 39:27, 28

e Kut 28:2
Kut 29:29
Law 16:4

f Law 16:16

g Law 16:20

h Law 16:18

i Law 16:24
1Yo 2:1, 2

j Law 23:31
Hes 29:7

k Kut 30:10
Ebr 9:7

SURA YA 17

l Law 3:1, 2
Law 7:11

Safu ya 2

a Law 3:3-5
Law 7:29-31

b Kum 32:17
Yos 24:14

c Kut 34:15
Kum 31:16

d Law 1:3
Kum 12:5, 6
Kum 12:13, 14

e Mwa 9:4
Law 3:17
Law 7:26
Law 19:26
1Sa 14:33
Mdo 15:20, 29

f Law 17:14
Kum 12:23

g Law 8:15
Law 16:18

h Mt 26:28
Ro 3:25
Ro 5:9
Efe 1:7
Ebr 9:22
Ebr 13:12
1Pe 1:2
1Yo 1:7
Ufu 1:5

i Kut 12:49

j Kum 12:23

Yehova damu ya dhahibu hizo kwenye mlango wa hema la mkutano na kuteketeza mafuta yake ili yafuke moshi ya kiwa harufu inayompendeza* Yehova.^a **7** Kwa hiyo hawapaswi tena kutoa dhahibu zao kwa roho waovu wenye umbo la mbuzi,^{*b} wanaofanya nao ukahaba.^c Hiyo itakuwa sheria ya kudumu kwa ajili yenu katika vizazi vyenu vyote.”

8 “Waambie hivi: ‘Mwisraeli yeyote au mgeni yeyote anayeishi miongoni mwenu atakayetoa dhahibu ya kuteketezwa au dhahibu yoyote **9** na kukosa kuleta kwenye mlango wa hema la mkutano ili kumtolea Yehova ni lazima auawe.^d

10 “Mwisraeli yeyote au mgeni yeyote anayeishi miongoni mwenu akila damu yoyote ile,^e kwa hakika nitamkataa* mtu anayekula damu, nami nitamwangamiza atoke miongoni mwa watu wake. **11** Kwa maana uhai wa kiumbe umo* katika damu,^f nami nimeitoa kwenye madhabahu^g ili mwitumie kufunika dhambi zenu, kwa maana damu ndiyo inayofunika dhambi^h kupitia uhai ulio ndani yake. **12** Ndiyo sababu nimewaambia Waisraeli hivi: “Hakuna yeyote kati yenu anayepaswa kula damu, na hakuna mgeni yeyote anayeishi miongoni mwenuⁱ anayepaswa kula damu.”^j

13 “Mwisraeli yeyote au mgeni yeyote anayeishi miongoni mwenu akiwinda na kumkamata mnyama wa mwituni au ndege anayeweza kuli-

17:6 *Au “inayomtuliza.” 17:7 *Tnn., “kwa wale mbuzi.” 17:10 *Tnn., “nitaukaza uso wangu dhidi ya.” 17:11 *Au “nafsi ya kiumbe imo.”

wa, ni lazima amwage damu yake^a chini na kuifunika kwa udongo. **14** Kwa maana uhai wa* kila kiumbe ni damu yake, kwa sababu uhai umo[#] ndani ya damu. Kwa hiyo, niliwaambia Waisraeli: “Hampaswi kula damu ya kiumbe yeyote kwa sababu uhai wa kila kiumbe umo katika damu yake. Mtu yeyote anayekula damu atauawa.”^b **15** Mtu yeyote, awe ni mwenyeji au mgeni, akila mnyama aliyepatikana amekufa au aliyeraruliwa na mnyama wa mwituni,^c basi ni lazima afue mavazi yake na kuoga kwenye maji,^d naye hatakuwa safi mpaka jioni. **16** Lakini asipofua mavazi yake na kuoga, atawajibika kwa sababu ya kosa lake.”^e

18 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Wambie Waisraeli hivi: ‘Mimi ni Yehova Mungu wenu.’^f **3** Msifanye kama wanavyofanya katika nchi ya Misri ambako mliishi, wala msifanye kama w navyofanya katika nchi ya Kanaani ambako nawapeleka.^g Msifuute sheria zao. **4** Mnapaswa kutekeleza sheria zangu,* nanyi mnapaswa kutii amri zangu na kuzifuata.^h Mimi ni Yehova Mungu wenu. **5** Ni lazima mshike amri zangu na sheria zangu;* yeyote anayefanya hivyo ataisi kupitia hizo.ⁱ Mimi ni Yehova.

6 “Hakuna mtu yeyote kati yenu anayepaswa kumkaribia mtu wake wa karibu wa ukoo ili kufanya naye ngono.*^j Mimi ni Yehova. **7** Usifanye ngono na baba yako wala mama

17:14 *Au “nafsi ya.” #Au “nafsi imo.” 18:4, 5 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.” 18:6 *Tnn., “kufunua uchi wake.”

SURA YA 17

a Kum 12:16
Kum 15:23

b Law 17:10, 11

c Kut 22:31
Kum 14:21

d Law 11:40

e Hes 19:20

SURA YA 18

f Mwa 17:7
Kut 6:7

g Kut 23:24
Law 20:23

h Law 20:22
Kum 4:1

i Lu 10:27, 28
Ro 10:5
Gal 3:12

j Law 20:17

Safu ya 2

a Mwa 35:22
Mwa 49:4
Law 20:11
Kum 27:20
2Sa 16:21
1Ko 5:1

b Law 20:17
Kum 27:22
2Sa 13:10-12

c Law 20:19

d Law 20:20

e Law 20:12

f Law 20:21
Kum 25:5
Mk 6:17, 18

g Law 20:14
Kum 27:23

yako. Yeye ni mama yako, usifanye naye ngono.

8 “Usifanye ngono na mke wa baba yako.^a Utamwaibisha baba yako.*

9 “Usifanye ngono na dada yako, awe ni binti ya baba yako au binti ya mama yako, awe amezaliwa katika nyumba ileile au amezaliwa nje.^b

10 “Usifanye ngono na binti ya mwana wako au binti ya binti yako, kwa sababu ni uchi wako mwenyewe.

11 “Usifanye ngono na binti ya mke wa baba yako, mtooto wa baba yako, kwa sababu ni dada yako.

12 “Usifanye ngono na dada ya baba yako. Ana uhusiano wa damu na baba yako.^c

13 “Usifanye ngono na dada ya mama yako, kwa sababu ana uhusiano wa damu na mama yako.

14 “Usimwaibishe* ndugu ya baba yako kwa kufanya ngono na mke wake. Mke huyo ni shangazi yako.^d

15 “Usifanye ngono na binti mkwe wako.^e Yeye ni mke wa mwana wako, usifanye naye ngono.

16 “Usifanye ngono na mke wa ndugu yako,^f kwa sababu utamwaibisha ndugu yako.*

17 “Usifanye ngono na mwanamke na binti yake.^g Usimchukue binti ya mwana wa mwanamke huyo na binti ya binti yake ili kufanya nao ngono. Wao ni watu wake wa karibu wa ukoo; hilo ni tendo chafu linalochukiza.*

18:8 *Tnn., “Ni uchi wa baba yako.”

18:14 *Tnn., “Usifunue uchi wa.” 18:16 *Tnn., “ni uchi wa ndugu yako.” 18:17 *Au “ni mwenendo wa aibu; mwenendo mchafu uliopotoka.”

18 “Usimchukue dada ya mke wako ili awe mke mwenz^a na kufanya naye ngono wakati mke wako angali hai.

19 “Usimkaribie mwana-mke wakati wa hedhi anapokuwa si safi ili kufanya naye ngono.^b

20 “Usifanye ngono na mke wa jirani yako* na hivyo kujichafua.^c

21 “Usikubali mtoto wako yeyote atolewe dhahihu kwa Moleki.^d Usilichafue jina la Mungu wako kwa njia hiyo.^e Mimi ni Yehova.

22 “Usilale na mwanamume kama vile unavyolala na mwanamke.^f Ni tendo linalochukiza.

23 “Mwanamume hapaswi kujichafua kwa kufanya ngono na mnyama; wala mwana-mke hapaswi kwenda kufanya ngono na mnyama.^g Kufanya hivyo kunakiuka sheria ya asili.

24 “Msijichafue kwa kufanya jambo lolote kati ya mambo hayo, kwa maana mataifa ninayoyafukuza kutoka mbele yenu yamejichafua kwa mambo hayo yote.^h

25 Kwa hiyo nchi si safi, nami nitaiadhibu kwa sababu ya dhambi yake, nayo nchi itawatapika wakaaji wake.ⁱ 26 Lakini ni lazima ninyi mzishike amri zangu na sheria zangu,^{*} msifanye jambo lolote kati ya mambo hayo yenye kuchukiza, awe ni mwenyeji au mgeni anayeishi miongoni mweni.^k 27 Kwa maana mambo hayo yote yenye kuchukiza yalifanywa na watu walioishi katika nchi hiyo kabla yenu,^l na

18:20 *Au “rafiki yako.” 18:26 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

SURA YA 18

a Mwa 30:15

b Law 15:19, 24
Law 20:18c Kut 20:14
Law 20:10
Kum 22:22
Met 6:29
Mt 5:27, 28
1Ko 6:9, 10
Ebr 13:4d Law 20:2
Kum 18:10
1Fa 11:7
2Fa 23:10

e Law 20:3

f Mwa 19:5
Law 20:13
Amu 19:22
Ro 1:26, 27
1Ko 6:9, 10
Yud 7g Kut 22:19
Law 20:15, 16h Law 20:23
Kum 18:12

i Mwa 15:16

j Law 20:22
Kum 4:1, 40

k Kut 12:49

l Kum 20:17, 18
2Fa 16:2, 3
2Fa 21:1, 2

Safu ya 2

a Law 18:3
Law 20:23
Kum 18:9

SURA YA 19

b Law 11:44
Isa 6:3
1Pe 1:15, 16
Ufu 4:8c Kut 20:12
Efe 6:2
Ebr 12:9d Kut 20:8, 11
Kut 31:13
Lu 6:5e Law 26:1
Zb 96:5
Hab 2:18
1Ko 10:14f Kut 20:4, 23
Kum 27:15

g Law 3:1

h Law 7:11, 12

i Law 7:17, 18

sasa nchi si safi. 28 Msifanye mambo hayo ili nchi isi-watapike kwa sababu ya kui-chafua kama itakavyoyatapika mataifa yaliyowatangu-lia. 29 Mtu yeyote akifanya jambo lolote kati ya mambo hayo yenye kuchukiza, wote wanaofanya mambo hayo ni lazima wauawe watoke miongoni mwa watu wao. 30 Ni lazima mtimize wajibu wenu kwangu kwa kutofuata desturi yoyote kati ya desturi yenye kuchukiza zilizofuatwa kabla yenu,^a ili msijichafue kwa desturi hizo. Mimi ni Yehova Mungu wenu.”

19 Yehova akaendelea ku-mwambia Musa: 2 “Wambie hivi Waisraeli wote: ‘Mnapaswa kuwa watakatifu, kwa sababu mimi, Yehova Mungu wenu, ni mtakatifu.^b

3 “Kila mmoja wenu anapaswa kumheshimu* mama yake na baba yake,^c nanyi mnapaswa kushika sabato zangu.^d Mimi ni Yehova Mungu wenu. 4 Msiigeukie miungu ya ubatili^e wala msijitengenezee miungu ya chuma.^f Mimi ni Yehova Mungu wenu.

5 “Mnaponitolea mimi Yehova dhahihu ya ushirika,^g mnapaswa kuitoa kwa njia itakayofanya mpate kibali.^h

6 Inapaswa kuliwa siku inayotolewa na siku inayofuata, lakini siku ya tatu, dhahihu inayobaki inapaswa kuteketezwa.ⁱ 7 Hata hivyo, ikiwa dhahihu yoyote inayobaki italiwa siku ya tatu, ni chukizo na haitakubaliwa. 8 Mtu anayeila ataadhibiwa kwa sababu ya kosa lake kwa maana

19:3 *Tnn., “kumwogopa.”

amechafua kitu kitakatifu cha Yehova, naye lazima auawe.

9 “Mnapovuna mashamba yenu, msivune kabisa ukingo wa mashamba yenu, nanyi msiokote masalio ya mavuno yenu.^a **10** Pia, msikusanye masalio ya mashamba yenu ya mizabibu wala msio-kote zabibu zilizoanguka chini. Waachieni maskini^{*b} na wageni. Mimi ni Yehova Mungu wenu.

11 “Msiibe,^c msidanganye,^d wala msitendeane kwa hila. **12** Msiape kwa uwongo kwa jina langu^e na hivyo kulichafua jina la Mungu wenu. Mimi ni Yehova. **13** Usimlaghai mwenzako^f wala kumnyang'anya vitu vyake.^g Usikae na mshahara wa kibarua usiku kucha mpaka asubuhi.^h

14 “Usimtukane^{*} kiziwi wala kuweka kizuizi mbele ya kipofu,ⁱ nawe ni lazima umwogope Mungu wako.^j Mimi ni Yehova.

15 “Usitoe hukumu isiyoye haki. Usiwabague maskini au kuwapendelea matajiri.^k Unapaswa kumhukumu mwenzako kwa haki.

16 “Usizunguezunguke kati ya watu wako ukieenea uchongezi.^l Usihatarishe uhai wa^{*} mwenzako.^m Mimi ni Yehova.

17 “Usimchukie ndugu yako moyoni mwako.ⁿ Lazima umkaripie mwenzako,^o usije ukashiriki dhambi yake.

18 “Usilipize kisasi^p wala usiwe na kinyongo dhidi ya wana wa watu wako, ni lazima umpende mwenzako kama

19:10 *Au “wanaoteseka.” **19:14** *Au “Usimlaani.” **19:16** *Tnn., “damu ya.”

SURA YA 19

a Lut 23:22
Kum 24:19

b Kum 15:7

c Kut 20:15
Efe 4:28

d Lut 6:2
Met 12:22
Efe 4:25

e Kut 20:7
Mt 5:33, 37
Yak 5:12

f Met 22:16
Mk 10:19

g Met 22:22

h Kum 24:15
Yer 22:13
Yak 5:4

i Kum 27:18

j Lut 25:17
Ne 5:15
Met 1:7
Met 8:13
1Pe 2:17

k Kut 23:3
Kum 1:16, 17
Kum 16:19
2Nya 19:6
Ro 2:11
Yak 2:9

l Zb 15:1, 3

m Kut 20:16
1Fa 21:13

n Met 10:18
1Yo 2:9
1Yo 3:15

o Zb 141:5
Met 9:8
Mt 18:15

p Met 20:22
Ro 12:19

Safu ya 2

a Mt 5:43, 44
Mt 22:39
Ro 13:9
Gal 5:14
Yak 2:8

b Kum 22:9

c Kum 22:11

d Lut 6:6, 7

e Kum 26:1, 2
Met 3:9

unavyojipenda mwenyewe.^a Mimi ni Yehova.

19 “Mnapaswa kushika sheria zangu: Usiwaache wanyama wako wa kufugwa wazaa na wanyama wengine wa aina tofauti. Usipande mbegu za aina mbili^b katika shamba lako, na usivae vazi lililoshonwa kwa nyuzi za aina mbili.^c

20 “Mwanamume akifanya ngono na kijakazi anayechumbiwa na mwanamume mwingine, na iwe kwamba kijakazi huyo hajakombolewa wala kuwekwa huru, wanapaswa kuadhibiwa. Hata hivyo, hawapaswi kuuawa, kwa sababu kijakazi huyo hakuwa amewe kwa huru. **21** Mwanamume huyo anapaswa kumletea Yehova dhabihu yake ya hatia kwenye mlango wa hema la mkutano, kondoo dume wa dhabihu ya hatia.^d **22** Kuhani atamtoa kondoo dume huyo wa dhabihu ya hatia ili kufunika dhambi ya mwanamume huyo mbele za Yehova, naye atasamehewa dhambi aliyo-tenda.

23 “Mtakapofika katika nchi hiyo na kupanda mti wote wa matunda, mnapaswa kuyaona matunda yake kuwa machafu na yaliyokatazwa.* Kwa miaka mitatu mkekatazwa kuyala.[#] Hayapaswi ku-liwa. **24** Lakini katika mwaka wa nne, matunda yake yote yatakuwa matakatifu, mtamtolea Yehova kwa shangwe.^e **25** Kisha katika mwaka wa tano, mnaweza kula matunda yake ili kuongeza mazao yake

19:23 *Tnn., “kuwa kama magovi yake.”
#Tnn., “Kwa miaka mitatu hayajatahiriwa.”

kwenye mavuno yenu. Mimi ni Yehova Mungu wenu.

26 “Msile kitu chochote kili-
lichu na damu.^a

“Msitafute ishara za uba-
shiri au kufanya uchawi.^b

27 “Msinyoe* masharafa
yenu au kuharibu kingo za
ndevu zenu.^c

28 “Msijikatekate mwilini
kwa ajili ya mtu aliyekufa,*^d
nanyi msijichanje chale. Mimi
ni Yehova.

29 “Usimwaibishe binti
yako kwa kumfanya kuwa ka-
haba,^e ili nchi isifanye ukaha-
ba na kujaa upotovu wa ma-
dili.^f

30 “Ni lazima mshike saba-
to zangu,^g nanyi mnapaswa
kuheshimu* mahali pangu pa-
takatifu. Mimi ni Yehova.

31 “Msiende kwa watu wa-
naowasiliana na roho,^h wala
msitafute ushauri kutoka kwa
wabashiriⁱ msije mkajichafua.
Mimi ni Yehova Mungu wenu.

32 “Unapaswa kuinuka
mbele ya kichwa chenye mvi,^j
na ni lazima umheshimu
mzee,^k nawe lazima umwogo-
pe Mungu wako.^l Mimi ni
Yehova.

33 “Mgeni akiishi nanyi ka-
tika nchi yenu, msimtese.^m

34 Mgeni anayeishi pamoja
nanyi mtamwona kama mwe-
nyeji;ⁿ nanyi lazima mumpen-
de kama mnavyojipenda
wenyewe, kwa maana mliku-
wa wageni nchini Misri.^o Mimi
ni Yehova Mungu wenu.

35 “Msitumie vipimo vya
uwongo kupima urefu, uzito,

19:27 *Au “Msipunguze; Msikate.”

19:28 *Au “kwa ajili ya nafsi iliyoku-
fa.” Neno la Kiebrania *ne'phesh* katika
andiko hili linamaanisha mtu aliyekufa.

19:30 *Tnn., “kuogopa.”

SURA YA 19

a Law 3:17
Law 17:13
Kum 12:23
Mdo 15:20, 29

b Kut 8:7
Kum 18:10-12
Gal 5:19, 20
Ufu 21:8

c Law 21:1, 5

d Kum 14:1

e Kum 23:17

f Ebr 13:4
1Pe 4:3

g Kut 20:10
Kut 31:13

h Law 20:6
Kum 18:10-12
1Nya 10:13
Isa 8:19

i Law 20:27
Mdo 16:16

j Met 16:31
Met 20:29

k Ayu 32:6
Met 23:22
1Ti 5:1

l Ayu 28:28
Met 1:7
Met 8:13
1Pe 2:17

m Kut 23:9

n Kut 12:49

o Kut 22:21

Safu ya 2

a Kum 25:13, 15
Met 20:10

b Met 11:1

c Law 18:5
Kum 4:6

SURA YA 20

d Law 18:21
Kum 18:10

e Eze 5:11

f Kum 13:6-9

g Kut 20:5

h Law 19:31
Kum 18:10-12
Gal 5:19, 20
Ufu 21:8

i Law 20:27
Mdo 16:16

au ujazo.^a **36** Mnapaswa ku-
tumia mizani sahihi, vipimo
sahihi, kipimo sahihi cha vitu
vikavu,* na kipimo sahihi cha
vitu vya majimaji.^b Mimi ni
Yehova Mungu wenu niliye-
watoa katika nchi ya Misri.
37 Kwa hiyo ni lazima mshike
masharti yangu yote na sheria
zangu zote,* mnapaswa kuzi-
fuata.^c Mimi ni Yehova.”

20 Yehova akaendelea ku-
mwambia Musa: **2** “Wa-
ambie hivi Waisraeli: ‘Mwa-
namume yeyote Mwisraeli na
mgeni yeyote anayeishi kati-
ka nchi ya Israeli atakaye-
mtoa mtoto wake dhabihu
kwa Moleki ni lazima aua-
we.^d Watu wote wanapaswa
kumuua kwa kumpiga mawe.

3 Mimi mwenyewe nitamka-
taa* mtu huyo, nami nitamwa-
ngamiza, kwa sababu ame-
mtoa mtoto wake dhabihu
kwa Moleki, ametia unajisi
mahali pangu patakatifu^e na
kulichafua jina langu takatifu.

4 Watu wakimwona mtu huyo
akimtoa mtoto wake dhabi-
hu kwa Moleki na wakatae ki-
makusudi kumuua mtu huyo,^f

5 basi mimi mwenyewe nita-
mkataa* mtu huyo pamoja na
familia yake.^g Nitamwangami-
za pamoja na wote waliojiu-
nga naye kufanya ukahaba na
Moleki.

6 “Kwa hakika nitamkataa
na kumwangamiza mtu yeyo-
te anayetafuta ushauri kutoka
kwa watu wanaowasiliana na
roho^h na pia wabashiriⁱ ili ku-

19:36 *Tnn., “kipimo sahihi cha efa.”
Angalia Nyongeza B14. *Tnn., “kipi-
mo sahihi cha hini.” Angalia Nyonge-
za B14. 19:37 *Tnn., “maamuzi yangu
yote ya hukumu.” 20:3, 5 *Tnn., “ni-
taukaza uso wangu dhidi ya.”

fanya ukahaba wa kiroho pamoja nao.^a

7 “Ni lazima mjitakase na kuwa watakatifu,^b kwa sababu mimi ni Yehova Mungu wenu.

8 Nanyi lazima mshike sheria zangu na kuzifuata.^c Mimi ni Yehova, ninayewatakasaa.^d

9 “Mtu yeyote anayemtukana* baba yake au mama yake lazima auawe.^e Kwa kuwa amemtukana baba yake au mama yake atakuwa na hatia kwa sababu ya kifo chake mwenyewe.[#]

10 “Ifuatayo ni sheria kuhusu mwanamume anayefanya uzinzi na mke wa mwanamume mwingine: Mwanamume anayefanya uzinzi na mke wa mwenzake lazima auawe; mwanamume huyo na mwanamke aliyefanya naye uzinzi lazima wauawe.^f 11 Mwanamume anayefanya ngono na mke wa baba yake amewaibisha baba yake.^g Ni lazima wote wawili wauawe. Watakuwa na hatia kwa sababu ya vifo vyao wenyewe.[#] 12 Mwanamume akifanya ngono na binti mkwe wake, wote wawili wanapaswa kuauwa. Wamekiuka sheria ya asili. Watakuwa na hatia kwa sababu ya vifo vyao wenyewe.^h

13 “Mwanamume akilala na mwanamume mwenzake kama vile mwanamume anavyolala na mwanamke, wote wawili wamefanya jambo linalochukiza.ⁱ Ni lazima wauawe. Watakuwa na hatia kwa sababu ya vifo vyao wenyewe.[#]

14 “Mwanamume akifanya ngono na mwanamke mwenye hedhi, mwanamume huyo na mwanamke huyo wamefunua mtiririko wa damu yake.^f Ni lazima wote wawili wauawe.

15 “Mwanamume akifanya ngono na dada ya mama yake au dada ya baba yake, kwa sababu kufanya hivyo ni kumwai-bisha mtu wako wa ukoo uliye na uhusiano wa damu naye.^g Wanapaswa kuadhibiwa kwa sababu ya kosa lao. 20 Mwanamume anayefanya ngono na

20:9 *Au “anayemlaani.” #Tnn., “damu yake itakuwa juu ya kichwa chake.” 20:11 *Tnn., “amefunua uchi wa baba yake.” 20:11-13, 16 #Tnn., “Damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao.”

SURA YA 20

a 1Nya 10:13

b Law 11:44
1Pe 1:15, 16

c Law 18:4
Mhu 12:13

d Kut 31:13
Law 21:8
1Th 5:23
2Th 2:13

e Kut 21:17
Kum 27:16
Met 20:20
Mt 15:4

f Kum 5:18
Kum 22:22
Ro 7:3
1Ko 6:9, 10

g Law 18:8
Kum 27:20

h Law 18:15, 29

i Mwa 19:5
Law 18:22
Amu 19:22
Ro 1:26, 27
1Ko 6:9, 10
Yud 7

Safu ya 2

a Law 18:17
Kum 27:23

b Law 21:9

c Kut 22:19
Kum 27:21

d Law 18:23

e Law 18:9
Kum 27:22

f Law 18:19

g Law 18:12, 13

14 “Mwanamume akimwoa mwanamke na afanye ngono na mama ya mwanamke huyo, ni tendo chafu linalochukiza.^a Anapaswa kuchomwa moto^b pamoja na wanawake hao, ili mwenendo huo mchafu unaochukiza usiendelee miongoni mwenu.

15 “Mwanamume akifanya ngono na mnyama lazima auawe, mnapaswa pia kumuua mnyama huyo.^c 16 Mwanamke akienda kufanya ngono na mnyama,^d ni lazima mu-muue mwanamke huyo pamoja na mnyama huyo. Lazima wauawe. Watakuwa na hatia kwa sababu ya vifo vyao wenyewe.[#]

17 “Mwanamume akifanya ngono na dada yake, binti ya baba yake au binti ya mama yake na kuona uchi wake na binti huyo pia aone uchi wake, ni jambo la aibu.^e Ni lazima wauawe mbele ya watu wote. Amemwai-bisha dada yake.* Anapaswa kuadhibiwa.

18 “Mwanamume akifanya ngono na mwanamke mwenye hedhi, mwanamume huyo na mwanamke huyo wamefunua mtiririko wa damu yake.^f Ni lazima wote wawili wauawe.

19 “Hupaswi kufanya ngono na dada ya mama yako au dada ya baba yako, kwa sababu kufanya hivyo ni kumwai-bisha mtu wako wa ukoo uliye na uhusiano wa damu naye.^g Wanapaswa kuadhibiwa kwa sababu ya kosa lao. 20 Mwanamume anayefanya ngono na

20:14 *Au “ni mwenendo wa aibu; mwenendo mchafu uliopotoka.” 20:17 *Tnn., “Amefunua uchi wa dada yake.”

mke wa ndugu ya baba yake amemwaibisha* ndugu ya baba yake.^a Wanapaswa kua-dhibiwa kwa sababu ya dhambi yao. Watakufa bila watoto. **21** Mwanamume aki-mchukua mke wa ndugu yake, ni jambo linalochukiza sana.^b Amemwaibisha ndugu yake.* Hawatazaa mtoto.

22 “Ni lazima mshike masharti yangu yote na sheria zangu zote^c na kuzifuata,^d ili nchi ninayowapa mwishi ndani yake isiwapitike.^e **23** Hampaswi kufuata sheria za mataifa ninayoyafukuza kuto-ka mbele yenu;^f kwa sababu yamefanya mambo hayo yote, nami ninayachukia kabisa mataifa hayo.^g **24** Ndiyo sababu niliwaambia: “Mtaimiliki nchi yao, nami nitawapa iwe miliki yenu, nchi inayotiririka maziwa na asali.^h Mimi ni Yehova Mungu wenu, nami nimewatenga na mataifa mengine.”ⁱ **25** Ni lazima mtofautishe mnyama aliye safi na asiye safi na ndege aliye safi na asiye safi;^j msinifanye niwachukie kwa kula mnyama au ndege au kiumbe yeyote anayetambaa niliyewaambia kwamba si safi.^k **26** Ni lazima muwe watakatifu mbele zangu, kwa sababu mimi, Yehova, ni mtakatifu,^l nami ninawatenga na mataifa mengine ili muwe watu wangu.^m

27 “Mwanamume au mwanamke yeyote ambaye anawasiliana na roho au ni mbashiri* lazima auawe.ⁿ Watu wanapaswa kuwaua kwa kuwapi-

20:20 *Tnn., “amefunua uchi wa.”
20:21 *Tnn., “Amefunua uchi wa ndugu yake.”
20:27 *Au “ana roho ya ubashiri.”

SURA YA 20

a Law 18:14

b Law 18:16
Kum 25:5c Kut 21:1
Kum 5:1

d Mhu 12:13

e Law 18:26, 28

f Law 18:3, 24
Kum 12:30g Law 18:27
Kum 9:5h Kut 3:17
Kut 6:8
Kum 8:7-9
Eze 20:6i Kut 19:5
Kut 33:16
1Fa 8:53
1Pe 2:9j Law 11:46, 47
Kum 14:4-20

k Law 11:43

l Law 19:2
Zb 99:5
1Pe 1:15, 16
Ufu 4:8

m Kum 7:6

n Kut 22:18
Law 19:31
Law 20:6
Kum 18:10-12
Ufu 21:8

Safu ya 2

SURA YA 21

a Hes 19:14

b Kum 14:1

c Law 19:27, 28

d Kut 29:44

e Law 18:21
Law 19:12
Law 22:32f Isa 52:11
1Pe 1:15, 16

g Law 19:29

h Kum 24:1
Eze 44:22

i Kut 28:41

j Kut 28:36
Law 11:45
Law 20:7, 8

ga mawe. Watakuwa na hatia kwa sababu ya vifo vyao wenyewe.”**

21 Yehova akaendelea kumwambia Musa: “Waa- mbie hivi wana wa Haruni, makuhani: ‘Mtu yeyote kati yenu asijichafue kwa kumgusa mtu aliyekufa* miongoni mwa watu wake.’^a **2** Lakini anaweza kufanya hivyo kwa ajili ya mtu wa karibu wa ukoo aliye na uhusiano wa damu naye, mama yake, baba yake, mwana wake, binti yake, ndugu yake, **3** na anaweza kujichafua kwa kumgusa dada yake wa karibu ikiwa ni bikira na hajaolewa. **4** Hapaswi kujichafua na kujitia unajisi kwa kumgusa mke wa mwanamume anayeto-ka katika ukoo wake. **5** Hawapaswi kunyoo upara^b au kukata ncha za ndevu zao au kujikatakata mwilini.^c **6** Wanapaswa kuwa watakatifu mbele za Mungu wao,^d nao hawapaswi kulichafua jina la Mungu wao,^e kwa sababu wanatoa dhabihu za Yehova zinazochomwa kwa moto, mkate wa* Mungu wao, lazima wawe watakatifu.^f **7** Hawapaswi kumwoa kahaba,^g mwanamke aliyetalikiwa na mume wake,^h kwa sababu kuhani ni mtakatifu mbele za Mungu wao. **8** Ni lazima umtakase kuhani,ⁱ kwa sababu ndiye anayetoa mkate wa Mungu wenu. Mnapaswa kumwona kuwa mtakatifu, kwa sababu mimi, Yehova, ninayewatakasaa ninyi, ni mtakatifu.^j

9 “Sasa binti ya kuhani akijichafua kwa kufanya ukaha-

20:27 *Tnn., “Damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao.”
21:1 *Au “kuigusa nafsi iliyokufa.”
21:6 *Au “chakula cha,” yaani, dhabihu.

ba, anamchafua baba yake. Binti huyo anapaswa kucho-mwa moto.^a

10 “Kuhani mkuu miongo-ni mwa ndugu zake, aliyetiwa mafuta kichwani^b na kuweka rasmi ili avae mavazi ya kuha-ni,^c anapaswa kutunza nywele zake na hapaswi kurarua ma-vazi yake.^d **11** Hapaswi ku-mkaribia mtu yeyote aliyeku-fa;^e hapaswi hata kujicha-fua kwa kungusa baba yake au mama yake ambaye ame-kufa. **12** Hapaswi kuondoka mahali patakatifu wala kucha-fua mahali patakatifu pa Mun-gu wake,^f kwa sababu ishara ya wakfu, yale mafuta ya Mun-gu wake yanayotumiwa kutia mafuta^g yako juu yake. Mimi ni Yehova.

13 “Ni lazima amwoe mwa-namke ambaye ni bikira,^h **14** Hapaswi kuoa mwanamke mjane, mwanamke aliyetaliki-wa, aliyenajisiwa, au kahaba; anapaswa kuoa mwanamke bi-kira miongoni mwa watu wake. **15** Hapaswi kucha-fua uzao wake* kati ya watu wake,ⁱ kwa sababu mimi ni Ye-hova, ninayemtakasa.”

16 Yehova akaendelea ku-mwambia Musa: **17** “Mwa-mbie hivi Haruni: ‘Mtu yeyote wa uzao wako* katika vizazi vyako vyote ambaye ana kaso-ro asikaribia mahali patakatifu ili kutoa mkate wa Mungu wake. **18** Mtu yeyote mwe-nye kasoro hapaswi kukaribia mahali patakatifu: mtu aliye kipofu au mlemavu au mwe-nye majeraha usoni* au mwe-

21:11 *Au “kuikaribia nafsi yoyote ili-yokufa.” 21:15 *Tnn., “mbegu yake.” 21:17 *Tnn., “mbegu yako.” 21:18 *Tnn., “pua iliyokatika.”

SURA YA 21

a Law 20:14

b Law 8:12

c Kut 28:2
Kut 29:29
Law 16:32d Mwa 37:34
Law 10:6e Hes 6:7
Hes 19:11, 14

f Law 10:7

g Law 8:12

h Eze 44:22

i Ezz 9:2

Safu ya 2

a Kum 23:1

b Law 2:10
Law 6:14, 16
Law 24:8, 9
Hes 18:9c Law 22:10
Hes 18:19

d Kut 30:6

e Kut 38:1

f Kut 25:8

g Kut 28:41

SURA YA 22

h Law 21:6

i Kut 28:38
Hes 18:32

nye kiungo kimoja kirefu zai-di, **19** au mtu aliyevunjika mguu au aliyevunjika mkono, **20** au kibyongo au mbiliki-mo,* au mtu mwenye jicho li-lilo na kasoro au mwenye ukuru-tu wa ngozi au mba au mwe-nye mapumbu yaliyoharibika.^a **21** Mtu yeyote wa uzao wa* kuhani Haruni ambaye ana kasoro hatakaribia mahali patakatifu ili kutoa dhahibu za Yehova zinazochomwa kwa moto. Kwa sababu ana kaso-ro, hapaswi kupakaribia ili ku-toa mkate wa Mungu wake. **22** Anaweza kula mkate wa Mungu wake kutoka kati ya vitu vitakatifu kabisa^b na ku-toka kati ya vitu vitakatifu.^c **23** Hata hivyo, hapaswi ku-karibia pazia^d wala madhaba-hu,^e kwa sababu ana kasoro mwilini; naye hapaswi kucha-fua mahali pangu patakatifu,^f kwa kuwa mimi ni Yehova, ni-nayewatakasa.”^g

24 Basi Musa akawaambia Haruni na wanawe, na Wais-raeli wote mambo hayo.

22 Yehova akaendelea ku-mwambia Musa: **2** “Mwa-mbie Haruni na wanawe kwa-mba wanapaswa kuwa waa-ngalifu kuhusu wanavyoshu-ghulikia* vitu vitakatifu vya Waisraeli, nao wasichafue jina langu takatifu^h kuhusu vitu wanavyotakasa kwa ajili ya-ngu.ⁱ Mimi ni Yehova. **3** Waa-mbie, ‘Katika vizazi vyenu vyote, mzao wenu yeyote asi-ye safi atakayekaribia vitu vitakatifu ambavyo Waisraeli wanavitakasa kwa ajili yangu,

21:20 *Au labda, “aliyekonda na ku-dhoofika.” 21:21 *Tnn., “mbegu ya.” 22:2 *Tnn., “kuhusu jinsi wanavyopa-swa kujitenga na.”

mimi, Yehova, ataangamizwa kutoka mbele zangu.^a Mimi ni Yehova. **4** Mzao yeyote wa Haruni mwenye ukoma^b au anayetokwa na umajimaji^c asile vitu vitakatifu mpaka atakapokuwa safi,^d wala mtu anayemgusa mtu yeyote aliyechafua kwa kugusa mtu aliyekufa,^e wala mtu anayetokwa na shahawa,^f **5** wala mtu anayemgusa kiumbe asiye safi anayeishi kwenye makundi makubwa^g wala mtu anayemgusa mtu asiye safi kwa sababu yoyote ile ambaye anaweza kumchafua.^h **6** Mtu anayegusa kitu chochote kati ya vitu hivyo hatakuwa safi mpaka jioni, naye hapaswi kula kitu chochote kitakatifu, badala yake anapaswa kuoga kwenye maji.ⁱ **7** Baada ya jua kutua, atakuwa safi, kisha anaweza kula baadhi ya vitu vitakatifu kwa sababu ni chakula chake.^j **8** Pia, hapaswi kujichafua kwa kula mnyama yeyote aliyepatikana amekufa au kiumbe yeyote aliyeraruliwa na mnyama wa mwituni.^k Mimi ni Yehova.

9 “Ni lazima watimize wajibu wao mbele zangu, wasije wakatenda dhambi kwa kukosa kutimiza wajibu huo na hivyo kufa kwa sababu walikuwa wakiuchafua. Mimi ni Yehova, ninayewatakasaa.

10 “Mtu asiye na idhini* haruhusiwi kula vitu vitakatifu.^l Hakuna mgeni wa kuhani au kibarua anayepaswa kula kitu chochote kitakatifu. **11** Lakini kuhani akimnunua mtu kwa pesa zake, mtu huyo ana-

SURA YA 22

a Law 7:20

b Law 13:2

c Law 15:2

d Law 14:2
Law 15:13e Law 21:1
Hes 19:11, 22

f Law 15:16

g Law 11:24, 43

h Law 15:7, 19

i Hes 19:6, 7

j Hes 18:11

k Kut 22:31
Law 17:15
Kum 14:21

l Kut 29:33

Safu ya 2

a Hes 18:11

b Law 10:14
Hes 18:19

c Law 5:15, 16

d Hes 18:32

e Hes 15:14, 16

f Law 7:16
Hes 15:3
Kum 12:5, 6g Law 1:3
Law 22:22h Kum 15:19, 21
Kum 17:1
Mal 1:8
Ebr 9:14
1Pe 1:19

weza kula vitu hivyo. Vilevile watumwa waliozaliwa katika nyumba yake wanaweza kula chakula chake.^a **12** Binti ya kuhani akiolewa na mwana-mume ambaye si kuhani,* hapaswi kula vitu vitakatifu vilivyotolewa mchango. **13** Lakini binti ya kuhani akiwa mjane au akitalikiwa na hana mtoto, naye arudi nyumbani kwa baba yake alikoishi kabla hajaolewa, anaweza kula kiasi fulani cha chakula cha baba yake;^b lakini mtu yeyote asiye na idhini* hapaswi kula chakula hicho.

14 “Mtu akila kitu kitakatifu bila kujua, ni lazima alipie kitu hicho na kuongeza sehemu ya tano ya thamani yake na kumpa kuhani.^c **15** Kwa hiyo makuhani hawapaswi kuchafua vitu vitakatifu ambavyo Waisraeli wanamtolea Yehova mchango^d **16** na hivyo kufanya Waisraeli waadhibiwe kwa sababu ya hatia ya kula vitu vyao vitakatifu; kwa maana mimi ni Yehova, ninayewatakasaa.”

17 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **18** “Waa-mbie hivi Haruni na wanawe na Waisraeli wote: ‘Mwanamume Mwisraeli au mgeni katika Israeli anapomtolea Yehova dhabihu ya kuteketezwa^e ili kutimiza nadhiri zake au kutoa toleo la hiari,^f **19** anapaswa kutoa ng’ombe dume asiye na kasoro,^g wanakondoo dume, au mbuzi ili apate kibali. **20** Hampaswi kutoa kitu chochote chenye kasoro,^h kwa sababu hamtapata kibali mkifanya hivyo.

22:12 *Au “ni mgeni.” 22:13 *Tnn., “mgeni yeyote,” yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni.

22:4 *Au “nafsi iliyokufa.” 22:10 *Tnn., “Mgeni,” yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni.

21 “Mtu akimtolea Yehova dhabihu ya ushirika^a ili kutimiza nadhiri au akiitoa ikiwa toleo la hiari, anapaswa kutoa mnyama asiye na kasoro kutoka katika mifugo yake au kundi lake, ili apate kibali. Mnyama huyo hapaswi kuwa na kasoro yoyote.

22 Hampaswi kumtoa dhabihu mnyama yeyote aliye kipofu, aliyevunjika, aliyekatawa, aliyegeruhiwa, mwenye uvimbe, vipele, au mba; hampaswi kumtolea Yehova yeyote kati ya wanyama hao au kumtolea Yehova dhabihu za aina hiyo kwenye madhabahu yake. **23** Mnaweza kumtoa ng’ombe dume au kondoo mwenye kiungo kimoja kirefu zaidi au kifupi sana kuwa toleo la hiari, lakini hatakuwaliwa mkimtoa kuwa dhabihu ya nadhiri. **24** Hampaswi kumtolea Yehova mnyama mwenye mapumbu yaliyominywa au kupondwa au kung’olewa au kukatwa; hampaswi kuwatoa dhabihu wanyama wa aina hiyo katika nchi yenu. **25** Nanyi hampaswi kupokea wanyama wa aina hiyo kutoka kwa mgeni na kuwatoa kuwa dhabihu kwa* Mungu wenu, kwa sababu wana kasoro na ni walemavu. Hawatakuwaliwa.”

26 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **27** “Ng’ombe dume au mwanakondoo dume au mbuzi akizaliwa, atakaa na mama yake kwa siku saba,^b lakini kuanzia siku ya nane atapokewa kwa kibali kuwa dhabihu, dhabihu kwa Yehova inayochoywa kwa moto. **28** Lakini hampaswi kumchinja ng’ombe dume

22:25 *Tnn., “mkate wa.”

au kondoo pamoja na watoto wake siku ileile.^a

29 “Mkimtolea Yehova dhabihu ya shukrani,^b mnapaswa kuitoa dhabihu hiyo ili mpate kibali chake. **30** Inapaswa kuliwa siku hiyohiyo. Hampaswi kuacha sehemu yoyote mpaka asubuhi.^c Mimi ni Yehova.

31 “Ni lazima mshike amri zangu na kuzifuata.^d Mimi ni Yehova. **32** Msilichafue jina langu takatifu,^e ni lazima nitakaswe miongoni mwa Waisraeli.^f Mimi ni Yehova, ninayewatakaswa,^g **33** ninayewatoa katika nchi ya Misri ili nijithibitisheshe kuwa Mungu wenu.^h Mimi ni Yehova.”

23 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Wambie hivi Waisraeli: ‘Sherehe za Yehova za majiraⁱ ambazo mnapaswa kutangaza^j ni makusanyiko matakatifu. Hizi ndizo sherehe zangu za majira:

3 “Mnaweza kufanya kazi kwa siku sita, lakini siku ya saba ni sabato ya pumziko kamili,^k kusanyiko takatifu. Hamtafanya kazi yoyote. Ni sabato kwa Yehova popote mnapoishi.^l

4 “Hizi ndizo sherehe za Yehova za majira, makusanyiko matakatifu ambayo mnapaswa kutangaza katika nyakati zilizopangwa za sherehe hizo: **5** Katika siku ya 14 ya mwezi wa kwanza,^m wakati wa jioni kabla ya giza kuingia* ni Pasakaⁿ ya Yehova.

6 “Siku ya 15 ya mwezi huo ni Sherehe ya Yehova ya Mikate Isiyo na Chachu.^o Kwa siku saba mnapaswa kula mikate

23:5 *Tnn., “katikati ya zile jioni mbili.”

SURA YA 22

a Law 3:1

b Kut 22:30

Safu ya 2

a Kut 23:19
Kum 22:6

b Law 7:12

c Law 7:15

d Law 19:37
Hes 15:40
Kum 4:40e Law 18:21
Law 19:12

f Law 10:3

g Kut 19:5
Law 20:8
Law 21:8h Kut 6:7
Law 11:45

SURA YA 23

i Kut 23:14
Law 23:37

j Hes 10:10

k Kut 16:30
Kut 20:10
Mdo 15:21

l Ne 13:22

m Hes 9:2, 3
Hes 28:16n Kut 12:3, 6
Kum 16:1
1Ko 5:7o Hes 28:17
1Ko 5:8

isiyo na chachu.^a **7** Siku ya kwanza, mtakuwa na kusanyiko takatifu.^b Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu. **8** Lakini kwa siku saba mta-
mtolea Yehova dhabihu inayochomwa kwa moto. Siku ya saba kutakuwa na kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu.”

9 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **10** “Waa-
mbie hivi Waisraeli: ‘Hatimaye mtakapoiingia katika nchi ninayowapa na kuvuna mazao yake, ni lazima mumletee kuhani tita la mavuno yenu ya kwanza.^c **11** Naye kuhani atatikisa tita hilo mbele za Yehova kwenda mbele na nyuma ili mpate kibali. Atalitikisa siku inayofuata siku ya Sabato. **12** Siku ambayo tita hilo linatikiswa, ni lazima mumtolee Yehova dhabihu ya kutekelezwa ya mwanakondoo dume wa mwaka mmoja asiye na kasoro. **13** Mtatoa pia sehemu mbili za kumi za kipimo cha efa* ya unga laini uliochanganywa na mafuta kuwa toleo la nafaka linalochomwa kwa moto, lenye harufu inayompendeza[#] Yehova. Pia mtatoa robo ya hini[^] ya divai kuwa toleo la kinywaji. **14** Msile mkate wowote, nafaka zilizo-
kaangwa, au nafaka zilizotoka kuvunwa, mpaka mtakapomtolea Mungu dhabihu zenu. Ni sheria ya kudumu katika vizazi vyenu vyote mahali popote mtakapoishi.

23:13, 17 *Sehemu mbili za kumi za efa zilikuwa sawa na lita 4.4 au kilogramu 2.6 hivi. Angalia Nyongeza B14. **23:13, 18** [#]Au “inayomtuliza.” **23:13** [^]Hini ilikuwa sawa na lita 3.67. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 23

a Kut 12:15
Kut 13:6
Kut 34:18

b Kut 12:16

c Hes 18:8, 12
Met 3:9
Eze 44:30
1Ko 15:20, 23

Safu ya 2

a Kut 34:22
Kum 16:9, 10

b Mdo 2:1

c Hes 28:26-31
Kum 16:16

d Law 7:11, 13

e Kut 23:16
Kut 34:22

f Hes 28:26, 27

g Law 4:23

h Law 3:1

i Law 7:34
Law 10:14
Hes 18:9
Kum 18:4
1Ko 9:13

j Hes 10:10

15 “Mnapaswa kuhesabu sabato saba kuanzia siku inayofuata siku ya Sabato, siku mnayotoa tita la toleo la kutikiswa.^a Yanapaswa kuwa majuma kamili. **16** Mtahesabu siku 50^b mpaka siku inayofuata Sabato ya saba, kisha mta-
mtolea Yehova toleo la nafaka iliyotoka kuvunwa.^c **17** Mnapaswa kuleta mikate miwili kutoka nyumbani ili iwe toleo la kutikiswa. Mikate hiyo inapaswa kuokwa kwa kutumia sehemu mbili za kumi za kipimo cha efa* ya unga laini. Inapaswa kuwa na chachu,^d ni mazao ya kwanza yaliyokomaa yanayotolewa kwa Yehova.^e **18** Nanyi mnapaswa kutoa mikate hiyo pamoja na wanakondoo dume saba wa mwaka mmoja wasio na kasoro, ng’ombe dume mmoja mchanga, na kondoo dume wawili.^f Watatolewa kwa Yehova wakiwa dhabihu ya kutekelezwa pamoja na toleo la nafaka na matoleo ya vinywaji, dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza[#] Yehova. **19** Pia mnapaswa kumtoa mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi^g na wanakondoo dume wawili wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya ushrika.^h **20** Kuhani atazitikisa dhabihu hizo kwenda mbele na nyuma pamoja na ile mikate ya mazao ya kwanza yaliyokomaa kama dhabihu ya kutikiswa mbele za Yehova, pamoja na wale wanakondoo dume wawili. Ni vitu vitakatifu vinavyotolewa kwa Yehova kwa ajili ya kuhani.ⁱ **21** Siku hiyo mtatangaza^j na kufanya kusanyiko takatifu. Hamtafanya kazi yoyote ngumu. Ni sheria

ya kudumu katika vizazi vyenu vyote mahali popote mnapoishi.

22 “Mnapovuna mashamba yenu, msivune kabisa ukiingo wa mashamba yenu, nanyi msikote masalio ya mavuno yenu.^a Waachieni maskini^{*b} na wageni.^c Mimi ni Yehova Mungu wenu.”

23 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **24** “Wambie hivi Waisraeli: ‘Siku ya kwanza ya mwezi wa saba, mtakuwa na pumziko kamili, mtaadhimisha kusanyiko takatifu litakalotangazwa kwa mlilo wa tarumbeta.^d **25** Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu, nanyi mtamtolea Yehova dhabihu inayochomwa kwa moto.’”

26 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **27** “Hata hivyo, siku ya kumi ya mwezi huo wa saba ni Siku ya Kufunika Dhambi.^e Mtakuwa na kusanyiko takatifu, nanyi mnapaswa kujitesa^{*f} na kumtolea Yehova dhabihu inayochomwa kwa moto. **28** Hampaswi kufanya kazi yoyote siku hiyo kwa sababu ni siku ya kufunika dhambi^g zenu mbele za Yehova Mungu wenu. **29** Mtu yeyote ambaye hatajitesa^{*siku} hiyo atauawa.^h **30** Nami nitamwangamiza mtu yeyote atakayefanya kazi yoyote siku hiyo. **31** Hampaswi kufanya kazi yoyote. Ni sheria ya kudumu katika vizazi vyenu vyote mahali popote mtakapoiishi. **32** Ni sabato ya pumzi-

23:22 *Au “wanaoteseka.” **23:27** *Kwa ujumla inaeleweka kwamba “kujitesa” kunamaanisha kujinyima kwa njia mbalimbali, kutia ndani kufunga. **23:29** *Au labda, “hatafanga.”

SURA YA 23

a Law 19:9
Kum 24:19
Ru 2:2, 3

b Isa 58:7

c Law 19:33

d Hes 10:10
Hes 29:1

e Kut 30:10
Law 25:9

f Law 16:29, 30
Hes 29:7

g Law 16:34
Ebr 9:12, 24-26
Ebr 10:10
1Yo 2:1, 2

h Hes 9:13
Hes 15:30

Safu ya 2

a Law 16:29-31
Law 23:27
Hes 29:7

b Kut 23:16
Hes 29:12
Kum 16:13
Ezr 3:4
Ne 8:14-18
Yoh 7:2

c Ne 8:18

d Kut 23:14
Kum 16:16

e Hes 28:26
Hes 29:7

f Law 1:3

g Law 2:1, 11

h Hes 15:5
Hes 28:6, 7

i Kut 16:23
Kut 20:8
Kut 31:13

j Kut 28:38
Hes 18:29

k Kum 12:11

l Hes 29:39
Kum 12:6
1Nya 29:9
2Nya 35:8
Ezr 2:68

m Kum 16:13

n Hes 29:12

ko kamili kwenu, nanyi mtaajitesa^a siku ya tisa ya mwezi huo wakati wa jioni. Mtaadhimisha sabato kuanzia jioni hiyo mpaka jioni inayofuata.”

33 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **34** “Wambie hivi Waisraeli: ‘Siku ya 15 ya mwezi huo wa saba mtamfanyia Yehova Sherehe ya Vibanda^{*siku} kwa siku saba.^b

35 Mtakuwa na kusanyiko takatifu siku ya kwanza, nanyi hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu. **36** Kwa siku saba mtamtolea Yehova dhabihu inayochomwa kwa moto. Siku ya nane mtakuwa na kusanyiko takatifu,^c nanyi mnapaswa kumtolea Yehova dhabihu inayochomwa kwa moto. Ni kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu.

37 “Hizo ndizo sherehe za Yehova za majira^d mnezopaswa kutangaza kuwa makusanyiko matakatifu^e ya kumtolea Yehova dhabihu hizi zinazochomwa moto: dhabihu ya kuteketezwa^f pamoja na toleo lake la nafaka^g na matoleo ya vinywaji^h kulingana na ratiba ya kila siku. **38** Mtazitoa pamoja na dhabihu zinazotolewa wakati wa sabato za Yehova,ⁱ pamoja na zawadi zenu,^j dhabihu zenu za nadhiri,^k na matoleo yenu ya hiari^l ambayo mnapaswa kumtolea Yehova.

39 Hata hivyo, siku ya 15 ya mwezi wa saba, baada ya kukusanya mavuno yenu, mnapaswa kufanya sherehe ya Yehova kwa siku saba.^m Siku ya kwanza ni ya pumziko kamili na siku ya nane ni ya pumziko kamili.ⁿ **40** Siku ya kwanza, mtachukua matunda ya

23:34 *Au “Vibanda vya Muda.”

miti yenu bora, matawi ya mitende,^a matawi ya miti yenye majani mengi na mierebi ya bondeni, nanyi mtashangilia^b mbele za Yehova Mungu wenu kwa siku saba.^c **41** Mtamfanyia Yehova sherehe hiyo kwa siku saba kila mwaka.^d Kwa kuwa ni sheria ya kudu mu katika vizazi vyenu vyote, mnapaswa kuisherehekea katika mwezi wa saba. **42** Mta-kaa katika vibanda kwa siku saba.^e Waisraeli wote wata-kaa katika vibanda, **43** ili vizazi vyenu vinavyokuja vijue kwamba^f niliwafanya Waisraeli wakae katika vibanda nilipowatoa nchini Misri.^g Mimi ni Yehova Mungu wenu.”

44 Basi Musa akawaambia Waisraeli kuhusu sherehe za Yehova za majira.

24 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Wamuru Waisraeli wakulettee mafuta safi ya zeituni zilizopondwa ili taa ziwake daima.^h **3** Katika hema la mkutano, nje ya pazia lililo karibu na sanduku la ushahidi, Haruni atahakikisha kwamba taa hizo zinawaka daima kuanzia jioni mpaka asubuhi mbele za Yehova. Hiyo ni sheria ya kudu mu katika vizazi vyenu vyote. **4** Haruni anapaswa kupanga taa hiyo kwa utaratibu kwenye kinara cha taaⁱ cha dhahabu safi mbele za Yehova daima.

5 “Utachukua unga laini na kuoka mikate 12 ya mviringo. Utatumia sehemu mbili za kumi za kipimo cha efa^j cha unga laini kuoka kila mkate. **6** Utaipanga mikate hiyo kwe-

24:5 *Sehemu mbili za kumi za efa zili-kuwa sawa na lita 4.4 au kilogramu 2.6 hivi. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 23

a Ne 8:15
Ufu 7:9

b Ne 8:10

c Kum 16:15

d Hes 29:12

e Kum 31:10, 11

f Kum 31:13
Zb 78:6

g Kut 12:37, 38
Hes 24:5

SURA YA 24

h Kut 27:20, 21
Hes 8:2

i Kut 25:31
Kut 39:33, 37
Ebr 9:2

Safu ya 2

a Kut 25:23, 24
1Fa 7:48

b Kut 40:22, 23
1Sa 21:4
Mk 2:25, 26

c Law 2:2
Law 6:15

d Hes 4:7
1Nya 9:32
2Nya 2:4

e Law 21:22
Law 22:10
1Sa 21:4, 6
Mt 12:3, 4
Lu 6:3, 4

f Law 6:14, 16

g Kut 12:38
Hes 11:4

h Kut 20:7
Kut 22:28
Law 19:12

i Kut 18:22

j Kut 18:15, 16
Hes 15:32, 34

k Hes 15:32, 35
Kum 17:7

nye safu* mbili juu ya meza ya dhahabu safi mbele za Yehova,^a kila safu itakuwa na mikate sita.^b **7** Unapaswa kuweka ubani safi juu ya kila safu, na mikate hiyo itakuwa dhahabu ya kumbukumbu*^c inayochomwa kwa moto mbele za Yehova. **8** Kila siku ya Sabato, anapaswa kupanga mikate hiyo mbele za Yehova kwa ukawaida.^d Ni agano linalodumu kati yangu na Waisraeli. **9** Itakuwa ya Haruni na wanawe,^e nao wataila mahali patakatifu,^f kwa sababu ni kitakatifu kabisa kwa ajili ya kuhani kutoka kwa dhahabu za Yehova zina-zochomwa kwa moto; itakuwa sheria ya kudumu.”

10 Siku moja, miongoni mwa Waisraeli, mwana fulani ambaye mama yake ni Mwisraeli na baba yake ni Mmisri^g alipigana na mwanamume Mwisraeli kambini. **11** Mwana huyo wa mwanamke Mwisraeli akaanza kulikufuru lile Jina* na kulitukana.^h Basi wakamleta kwa Musa.ⁱ Kumbe mama yake alikuwa Shelomithi, binti ya Dibri wa kabila la Dani. **12** Kwa hiyo wakamtia kifungoni mpaka walipojulishwa uamuzi wa Yehova.^j

13 Kisha Yehova akamwambia Musa: **14** “Mtoeni nje ya kambi yule aliyelitukana, na wale wote waliomsikia wanapaswa kuweka mikonao yao juu ya kichwa chake, kisha Waisraeli wote watampiga mawe.^k **15** Nawe utawaa-ambia hivi Waisraeli: ‘Mtu yeyote akimtukana Mungu wake,

24:6 *Au “tabaka.” **24:7** *Au “itakuwa sehemu ya ukumbusho (uwakilishi) wake.” **24:11** *Yaani, jina Yehova, kulingana na mstari wa 15 na 16.

atawajibika kwa sababu ya dhambi yake. **16** Kwa hiyo yule aliyelitukana jina la Yehova lazima auawe.^a Kwa hakika kusanyiko lote linapaswa kupiga mawe. Mgeni anapaswa kuuawa sawasawa na mwenyeji kwa sababu ya kulitukana lile Jina.

17 “Mtu anayemua mwanadamu mwenzake* lazima auawe.^b **18** Mtu yeyote anayepiga na kumuua mnyama wa kufugwa* anapaswa kulipa fidia, uhai kwa uhai.[#] **19** Mtu akimjeruhi mwanadamu mwenzake, basi anapaswa kutendewa jambo alilotenda.^c **20** Mfupa uliovunjika kwa mfupa uliovunjika, jicho kwa jicho, jino kwa jino, atajeruhiwa kama alivyomjeruhi mwenzake.^d **21** Mtu anayepiga na kumuua mnyama anapaswa kulipa fidia,^e lakini mtu anayepiga na kumuua mwanadamu anapaswa kuuawa.^f

22 “Sheria itakuwa moja kwenu, iwe ni mgeni au mwenyeji,^g kwa sababu mimi ni Yehova Mungu wenu.”

23 Basi Musa akawaambia Waisraeli mambo hayo, wakamtoa nje ya kambi yule aliyelitukana lile Jina, wakampiga mawe.^h Kwa hiyo Waisraeli wakafanya kama Yehova alivyomwamuru Musa.

25 Yehova akaendelea kumwambia Musa kwenye Mlima Sinai, **2** “Waambie hivi Waisraeli: ‘Hatimaye mtakapoiingia katika nchi ninayowapa,’ nchi hiyo itashika sabato ya Yehova.ⁱ **3** Kwa mia-

24:17 *Au “anayeuua nafsi yoyote ya mwanadamu.” **24:18** *Au “anayepiga na kuuua nafsi ya mnyama.” #Au “nafsi kwa nafsi.”

SURA YA 24

a Kum 5:11

b Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:31
Kum 19:11-13

c Kut 21:23, 24

d Kum 19:21
Mt 5:38

e Kut 22:1

f Mwa 9:6
Kut 21:12g Kut 12:49
Law 17:10
Law 19:34
Hes 9:14
Hes 15:16h Hes 15:33, 36
Kum 17:7

SURA YA 25

i Mwa 15:16

j Law 26:34
2Nya 36:20, 21

Safu ya 2

a Kut 23:10, 11

b Law 16:30
Law 23:27, 28c Isa 61:1, 2
Lu 4:18, 19
Ro 8:20, 21d Law 27:24
Hes 36:4
Kum 15:1

ka sita mtapanda mbegu katika mashamba yenu, mtapunguza matawi ya mizabibu yenu, na kuvuna mazao ya nchi.^a **4** Lakini katika mwaka wa saba nchi itakuwa na pumziko kamili la sabato, sabato ya Yehova. Hampaswi kupanda mbegu wala kupunguza matawi ya mizabibu yenu. **5** Hampaswi kuvuna nafaka yoyote inayoota yenyewe baada ya mavuno, nanyi hampaswi kuchuma zabibu kutoka kwenye mizabibu yenu ambayo haijapunguza matawi. Ni lazima nchi iwe na mwaka wa pumziko kamili. **6** Hata hivyo, mnaweza kula mazao yanayoota nchini mwaka huo wa sabato, yaani, mtayala ninyi wenyewe, na pia watumwa wenu wa kike na wa kiume, vibarua wenu, wageni wanaoishi nanyi, **7** na pia wanyama wenu wa kufugwa na wanyama wa mwituni walio katika nchi yenu. Mnaweza kula mazao yote nchini.

8 “Mtahesabu miaka saba ya sabato, miaka saba mara saba, jumla ya miaka 49. **9** Kisha mtapiga pembe kwa sauti kubwa katika mwezi wa saba, siku ya kumi ya mwetzi huo; katika Siku ya Kufunika Dhambi^b mnapaswa kupiga pembe katika nchi yenu yote. **10** Mtautakasa mwaka wa 50 na kutangaza uhuru kwa wakaaji wote nchini.^c Utakuwa Mwadhimisho wa Miaka 50, na kila mmoja atarudi kwenye urithi wake na kila mmoja wenu atarudi kwa familia yake.^d **11** Mwaka huo utakuwa mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50. Hamtapanda mbegu wala kuvuna nafaka iliyoota yenyewe wala kuchuma

zabibu kutoka kwenye mizabibu ambayo haijapunguzwa matawi.^a **12** Kwa maana ni Mwadhimisho wa Miaka 50, ni mwaka mtakatifu kwenu. Mnaweza kula tu mazao yanayoota yenyewe nchini.^b

13 “Katika mwaka huo wa 50, kila mmoja wenu anapaswa kurudi kwenye urithi wake.^c **14** Ukiuza au kununua chochote kutoka kwa mwenzako, usimpunje.^d

15 Bei ya unachonunua inapaswa kulingana na idadi ya miaka ambayo imepita baada ya Mwadhimisho wa Miaka 50, naye anapaswa kukuuzia kulingana na idadi ya miaka inayobaki ya mazao.^e

16 Ikiwa miaka inayobaki ni mingi, anaweza kuongeza bei, na ikiwa ni michache anapaswa kupunguza bei kwa sababu anakuuzia idadi ya mazao utakayovuna. **17** Hakuna yeyote kati yenu anayepaswa kumpunja mwenzake,^f ni lazima mmwogope Mungu wenu,^g kwa sababu mimi ni Yehova Mungu wenu.^h **18** Mkishika amri zangu na kufuata sheria zangu,^{*} mtaishi kwa usalama nchini.ⁱ **19** Nchi itazaa mazao yake,^j nanyi mtakula na kushiba na kuishi humo kwa usalama.^k

20 “Iwapo mtauliza: “Tutakula nini katika mwaka wa saba tusipopanda mbegu au kuvuna mazao yetu?”^l **21** Nitaamuru baraka zangu zije juu yenu katika mwaka wa sita, nayo nchi itazaa mazao ya kutosha kwa miaka mitatu.^m **22** Nanyi mtapanda mbegu mwaka wa nane na kula ma-

25:18 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

SURA YA 25

a Law 25:5

b Kut 23:11
Law 25:6c Law 25:29, 30
Law 27:24d 1Sa 12:3
Met 14:31

e Law 27:18

f Law 19:13
Met 22:22g Law 25:43
Met 1:7
Met 8:13

h Isa 33:22

i Kum 12:10
Zb 4:8
Met 1:33

j Zb 67:6

k Law 26:3-5

l Law 25:4, 5
Mt 6:25m Mwa 26:12
Kum 28:8
Mal 3:10

Safu ya 2

a 1Fa 21:3

b Zb 24:1

c 1Nya 29:15

d Ru 2:20
Ru 4:4-6

e Law 25:50

f Law 27:24

g Law 25:10, 13

h Law 25:25-27

vuno ya miaka iliyotangulia mpaka mwaka wa tisa. Mtakula mavuno hayo mpaka mtakapovuna mwaka huo.

23 “Kwa hiyo ardhi haipaswi kuuzwa kwa muda wa kudumu,^a kwa sababu nchi ni yangu.^b Kwa maana ninyi ni wageni na wahamiaji machoni pangu.^c **24** Katika nchi yote mnayomiliki, mtakuwa na haki ya kukomboa* ardhi mliyouza.

25 “Ikiwa ndugu yako atakuwa maskini na hivyo alazimike kuuza sehemu fulani ya urithi wake, basi mkombozi ambaye ni mtu wake wa karibu wa ukoo atakuja na kununua sehemu iliyouzwa na ndugu yake.^d **26** Ikiwa mtu hana mkombozi lakini anapata ufanisi na kupata uwezo wa kukomboa, **27** anapaswa kuhesabu thamani yake kulingana na miaka iliyopita tangu alipoiuza na kumrudishia yule aliyeinunua kiasi kinachobaki. Kisha atarudi kwenye urithi wake.^e

28 “Lakini ikiwa hana uwezo wa kukomboa sehemu aliyouza, sehemu hiyo itabaki mikononi mwa mnunuzi mpaka mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50;^f kisha atarudishiwa sehemu hiyo mwaka huo, naye atarudi kwenye urithi wake.^g

29 “Mtu akiuza nyumba yake iliyo katika jiji lililozingirwa na ukuta, anaweza kukomboa mwaka mmoja tangu alipoiuza; kwa mwaka mzima atakuwa na haki ya kukomboa.^h **30** Lakini ikiwa haitakombolewa katika muda wa mwaka mzima, nyumba hiyo

25:24 *Au “kununua tena.”

iliyozingirwa na ukuta itakuwa mali ya kudumu ya yule aliyeinunua katika vizazi vya-ke vyote. Haipaswi kurudishwa wakati wa Mwadhimisho wa Miaka 50. **31** Hata hivyo, nyumba zilizo katika vijiji ambavyo havijazingirwa na ukuta zinapaswa kuhesabiwa kama mashamba. Zinaweza kukombolewa, nazo zinapaswa kurudishwa wakati wa Mwadhimisho wa Miaka 50.

32 “Lakini Walawi wana haki ya kukomboa nyumba zao zilizo katika majiji yao^a wakati wowote. **33** Mlawi asipokomboa nyumba yake, nyumba hiyo iliyozwa katika jiji la Walawi itarudishwa wakati wa Mwadhimisho wa Miaka 50,^b kwa sababu nyumba zilizo katika majiji ya Walawi ni urithi wao miongoni mwa Waisraeli.^c **34** Istitoshe, malisho^d yanayozunguka majiji yao hayapaswi kuuza, kwa sababu ni urithi wao wa kudumu.

35 “Ikiwa ndugu yako aliyekaribu nawe amekuwa maskini na hawezi kujiruzuku, unapaswa kumsaidia,^e kama ambavyo ungemsaidia mgeni na pia mhamiaji,^f ili aendelee kuwa hai kama wewe. **36** Usimtoze riba au kujipatia faida kutoka kwake.^g Ni lazima umwogope Mungu wako,^h na ndugu yako ataendelea kuwa hai kama wewe. **37** Usimkopeshe pesa kwa ribaⁱ au kumpa chakula ili upate faida. **38** Mimi ni Yehova Mungu wenu, niliyewatoa nchini Misri^j ili kuwapa nchi ya Kanaani, ili nijithibitisha kuwa Mungu wenu.^k

39 “Ikiwa ndugu yako anayeishi karibu nawe amelazimi-

SURA YA 25

a Hes 35:2, 8

b Law 25:28

c Hes 18:20
Hes 35:2, 4
Kum 18:1d Hes 35:7
Yos 14:4e Kum 15:7
Zb 41:1
Zb 112:5
Met 3:27
Met 19:17
Mdo 14:7
Mdo 11:29
ITI 6:18
IYo 3:17f Kut 22:21
Kut 23:9
Law 19:34
Kum 10:18g Kut 22:25
Kum 23:19
Zb 15:5
Met 28:8

h Met 8:13

i Kum 23:20
Lu 6:34, 35j Kut 20:2
IFa 8:51

k Kut 6:7

Safu ya 2

a Kut 21:2
Kum 15:12

b IFa 9:22

c Law 25:53

d Kut 21:3
Law 25:10e Kut 1:13, 14
Kut 19:5
Law 25:55f Kut 3:7
Efe 6:9
Kol 4:1g Law 25:17
Mhu 12:13h Kut 12:38
Yos 9:21

i Law 25:39, 43

ka kujiuza kwako^a kwa sababu amekuwa maskini, usimlazimishe akutumikie kama mtumwa.^b **40** Unapaswa kumtendea kama kibarua,^c kama mhamiaji. Atakutumikia mpaka wakati wa Mwadhimisho wa Miaka 50. **41** Kisha atakuacha, yeye na watoto^{*} wake, na kurudi kwa watu wake wa ukoo. Anapaswa kurudi kwenye urithi wa mababu zake.^d **42** Kwa maana wao ni watumwa wangu niliowatoa nchini Misri.^e Hawapaswi kujiuza kama mtumwa anavyozwa. **43** Usimtendea kwa ukatili,^f ni lazima umwogope Mungu wako.^g **44** Utawachuka watumwa wa kike na wa kiume kutoka katika mataifa jirani, unaweza kumnunua mtumwa wa kiume au wa kike kutoka katika mataifa hayo. **45** Pia unaweza kununua watumwa kutoka miongoni mwa wana wa wageni wanaoishi nawe^h na kutoka kati ya watu wa familia zao waliozaliwa katika nchi yenu, nao watakuwa mali yako. **46** Unaweza kuwarithisha kwa wana wako ili wawe mali yao ya kudumu. Unaweza kuwatumia watumwa hao kama wafanyakazi, lakini usiwatende ndugu zako Waisraeli kwa ukatili.ⁱ

47 “Lakini ikiwa mgeni au mhamiaji miongoni mwenu amekuwa tajiri na ndugu yako amekuwa maskini kando yake na hivyo analazimika kujiuza kwa mgeni au mhamiaji huyo anayeishi miongoni mwenu, au kwa mtu wa ukoo wa mgeni huyo, **48** ndugu yako ambaye amejiuza ataendelea

25:41 * Tnn., “wana.”

kuwa na haki ya ukombozi hata baada ya kujiuza. Mmoja wa ndugu zake anaweza kumkomboa,^a **49** au anaweza kukombolewa na ndugu ya baba yake au binamu yake, au na mtu yeyote wa karibu wa ukoo,* yaani, mtu wa familia yake.

“Au anaweza kujikomboa mwenyewe akipata utajiri.^b **50** Yeye pamoja na mtu aliye-mnunua watahesabu idadi ya miaka tangu mwaka aliojiuza mpaka mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50,^c na bei ya kukombolewa kwake itahesabiwa kulingana na idadi hiyo ya miaka.^d Muda aliofanaya kazi utapimwa kama muda wa mtu anayefanya kazi ya kibarua.^e **51** Ikiwa miaka inayobaki ni mingi, anapaswa kulipa bei yake ya ukombozi kulingana na miaka inayobaki. **52** Lakini ikiwa ni miaka michache tu inayobaki kabla ya mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50, anapaswa kuhesabu mwenyewe bei yake ya ukombozi na kulipa kulingana na miaka inayobaki. **53** Ataendelea kumtumikia kama kibarua mwaka baada ya mwaka; mnapaswa kuhakikisha kwamba yule aliyemnunua hamtendei kwa ukatili.^f **54** Hata hivyo, ikiwa hawezi kujinunua kulingana na masharti hayo, ataachiliwa huru pamoja na watoto* wake wakati wa Mwadhimisho wa Miaka 50.^g

55 “Kwa maana Waisraeli ni watumwa wangu mwenyewe. Ni watumwa wangu niliowatoa nchini Misri.^h Mimi ni Yehova Mungu wenu.

25:49 *Au “mwenye uhusiano wa damu naye.” 25:54 *Tnn., “wana.”

SURA YA 25

a Law 25:25

b Law 25:26, 27

c Law 25:10

d Law 25:15, 16

e Kum 15:18

f Law 25:40, 43
Kol 4:1

g Kut 21:3

h Kut 20:2
Law 25:42

Safu ya 2

SURA YA 26

a Kut 20:4
Law 19:4
Mdo 17:29
1Ko 8:4

b Kum 5:8

c Hes 33:52

d Da 3:18
1Ko 10:14e Kum 11:13-15
Mhu 12:13f Kum 28:12
Isa 30:23
Eze 34:26
Yoe 2:23g Zb 67:6
Zb 85:12

h Law 25:18

i 1Nya 22:9
Zb 29:11
Hag 2:9

j Mik 4:4

k Kum 28:7
Yos 23:10
Amu 7:15, 16
Amu 15:15, 16
1Nya 11:20

l Kum 28:4

m Kut 6:4

26 “Msijitengenezee miungu ya ubatili^a wala sanamu ya kuchongwa^b au nguzo takatifu, nanyi msichonge sanamu ya mawe^c katika nchi yenu na kuiinamia;^d kwa maana mimi ni Yehova Mungu wenu. **2** Mnapaswa kushika sabato zangu na kuheshimu* mahali pangu patakatifu. Mimi ni Yehova.

3 “Mkiendelea kufuata sheria zangu na kushika amri zangu na kuzitekeleza,^e **4** nitawaletea mvua katika majira yanayofaa,^f nayo nchi itazaa kwa wingi,^g na miti ya matunda itazaa matunda mengi. **5** Majira yenu ya kupura nafaka yataendelea mpaka wakati wa kuvuna zabibu, na wakati wa kuvuna zabibu utaendelea mpaka wakati wa kupanda; nanyi mtakula mkate na kushiba na kuishi kwa usalama katika nchi yenu.^h **6** Nitaleta amani nchini,ⁱ nanyi mtalala na hakuna yeyote atakayewaogopesha;^j nami nitawaondoa nchini wanyama wote wakali wa mwituni, na hakuna mtu yeyote atakayewashambulia kwa upanga katika nchi yenu. **7** Nanyi hakika mtawakimbiza maadui wenu na kuwaua kwa upanga. **8** Watu watano kati yenu watawakimbiza maadui 100, na 100 watawakimbiza 10,000; mtawaua maadui wenu kwa upanga.^k

9 “Nitawabariki* na kuwafanya mzaane na kuongezeka,^l nami nitatimiza agano nililofanya pamoja nanyi.^m **10** Wakati wa mavuno mtakuwa bado mnakula mavuno ya zamani ya mwaka uliotangu-

26:2 *Au “kuogopa.” 26:9 *Au “Nitawakazia fikira.”

lia, mtahitaji kuondoa mavuno hayo ya zamani ili mpa-te nafasi ya mavuno mapya. **11** Nami nitaweka hema langu la ibada kati yenu,^a nami sitawakataa. **12** Nitatembea kati yenu na kuwa Mungu wenu,^b nanyi mtakuwa watu wangu.^c **13** Mimi ni Yehova Mungu wenu, niliyewatoa katika nchi ya Misri ili msiendeleo kuwa watumwa wao, nami nikavunja nira yenu na kuwafanya mtembee vichwa vyenu vikiwa vimeinuliwa.*

14 “Lakini msiponisikiliza au kushika amri hizo zote,^d **15** mkikataa masharti yangu,^e mkichukia sheria zangu,^f na kuvunja agano langu kwa kuacha kushika amri zangu zote,^f **16** basi, mimi nitawatendea mambo haya: nitawaadhibu kwa taabu, kwa kifua kikuu na homa kali, na kufanya macho yenu yadhoo-fike na uhai wenu uzorote.* Mtapanda mbegu zenu bure, kwa maana maadui wenu watazila.^g **17** Nitawakataa,* nanyi mtashindwa na maadui wenu;^h na wale wanaowachukia ninyi watawakanyagakanya,ⁱ nanyi mtakimbia bila kukimbizwa na mtu.^j

18 “Hata mambo hayo yasipowafanya mnisikilize, nitalezimika kuwaadhibu mara saba zaidi kwa sababu ya dhambi zenu. **19** Nitakivunja kiburi chenu cha ukaidi na kufanya mbingu zenu ziwe kama chuma^k na nchi yenu kama shaba. **20** Mtapoteza nguvu zenu bure, kwa maana nchi

26:13 *Tnn., “mtembee wima.” **26:15** *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.” **26:16** *Au “nafsi yenu izarote.” **26:17** *Tnn., “Nitaukaza uso wangu dhidi yenu.”

SURA YA 26

a Kut 25:8
Eze 37:26
Ufu 21:3

b Kum 23:14

c Kut 6:7
2Ko 6:16

d Kum 28:15

e 2Fa 17:15

f Kut 24:7
Kum 31:16
Ebr 8:9

g Kum 28:22, 33
Amu 6:3

h Kum 28:15, 25
Amu 2:14
1Sa 4:10

i Zb 106:41
Omb 1:5

j Law 26:36

k Kum 11:17
1Fa 17:1

Safu ya 2

a Yer 12:13
Hag 1:6, 10

b Kum 32:24
Yer 15:3

c Eze 5:17

d Amu 5:6
Isa 33:8
Zek 7:14

e Isa 1:16
Yer 2:30
Yer 5:3

f Kut 24:7

g Kum 28:21
Yer 24:10
Amo 4:10

h Amu 2:14
1Sa 4:10

i Eze 5:16

j Eze 4:16

k Isa 9:20
Mik 6:14
Hag 1:6

l Yer 21:5

m Kum 28:53
2Fa 6:29
Yer 19:9

Omb 4:10
Eze 5:10

n 2Nya 34:3
Isa 27:9

yenu haitazaa mazao yake,^a na miti iliyo nchini haitazaa matunda.

21 “Lakini mkiendelea kunipinga na kukataa kunisikiliza, ndipo mimi nitalazimika kuwapiga mara saba zaidi, kulingana na dhambi zenu. **22** Nitaleta wanyama wa mwituni kati yenu,^b nao watawau watoto wenu,^c wataangamiza mifugo yenu na kupunguza idadi yenu, na barabara zenu hazitakuwa na watu.^d

23 “Msipokubali nidhamu yangu^e licha ya mambo hayo, nanyi kwa ushupavu mtembee kwa kunipinga, **24** basi mimi pia nitawapinga, nami mwenyewe nitawapiga mara saba kwa sababu ya dhambi zenu. **25** Nitaleta dhidi yenu upanga unaolipiza kisasi kwa sababu ya kulivunja agano langu.^f Hata mkikusanyika katika majiji yenu, nitaleta magonjwa katikati yenu^g na kuwatia mikononi mwa adui.^h **26** Nitakapoharibu hifadhi yenu ya* mikate,ⁱ wanawake kumi wataoka mikate kwenye jiko moja tu na kuwapimia mikate kwa mizani;^j nanyi mtakula lakini hamtashiba.^k

27 “Na ikiwa hamtanisikiliza, nanyi mkinipinga kwa ushupavu licha ya mambo hayo, **28** nitazidisha upinzani wangu dhidi yenu,^l na mimi mwenyewe nitawaadhibu mara saba kwa sababu ya dhambi zenu. **29** Basi mtalezimika kula nyama ya wana wenu na nyama ya mabinti wenu.^m **30** Nitaharibu mahali penu patakatifu palipo juuⁿ

26:26 *Tnn., “fito zenu za.” Labda ni fito zilizotumiwa kuhifadhia mikate.

na kuvikatakata vinara vyenu vya uvumba, nami nitarundi-ka mizoga yenu juu ya mizoga ya sanamu zenu zenye kuchukiza,*^a nami nitawachukia na kuwaacha.^b **31** Nitayaa-ngamia majiji yenu kwa upanga^c na kuharibu mahali penu patakatifu, nami sitasikia harufu inayopendeza* ya dhahabu zenu. **32** Mimi mwenyewe nitaifanya nchi yenu iwe ukiwa,^d na maadui wenu watakaoshi humo watashangazwa na hali yake.^e **33** Nitawatawanya miongoni mwa mataifa,^f nitachomoa upanga nanyi mtakimbizwa;^g na nchi yenu itaharibiwa, na majiji yenu yatabaki ukiwa.^h

34 “Wakati huo nchi italipa sabato zake siku zote itakapokuwa ukiwa, mtakapokuwa katika nchi ya maadui wenu. Wakati huo nchi itapumzika,* kwa maana ni lazima ilipe sabato zake.ⁱ **35** Siku zote itakapokuwa ukiwa itapumzika, kwa sababu haikupumzika wakati wa sabato zenu mlipokuwa mkiishi humo.

36 “Nitajaza hisia ya kuka-ta tamaa mioyoni mwa wale watakaobaki/ katika nchi za maadui wao; na sauti ya jani linalopeperushwa na upepo itawafanya wakimbie, nao watakimbia kama mtu anayeu-kiambia upanga na kuanguka bila kukimbizwa na yeyote.^k **37** Watajikwaa na kuangukiana kama watu wanao-kimbia upanga, hata ingawa hakuna anayewakimbiza. Hamtaweza kuwashinda maadui

26:30 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau. **26:31** *Au “inayotuliza.” **26:34** *Au “itashika sabato.”

SURA YA 26

- a 1Fa 13:2
2Fa 23:8, 20
Eze 6:5
b Zb 78:58, 59
c 2Fa 25:9, 10
2Nya 36:17
Ne 2:3
Isa 1:7
Yer 4:7
d Yer 9:11
e Kum 28:37
Kum 29:22-24
Yer 18:16
Omb 2:15
Eze 5:15
f Zb 44:11
g Yer 9:16
Eze 12:14
h Zek 7:14
i 2Nya 36:20, 21
j Isa 24:6
k Law 26:17
Isa 30:17

Safu ya 2

- a Yos 7:12
Amu 2:14
Yer 37:10
b Kum 4:27
Kum 28:48
Yer 42:17
c Kum 28:65
d Kut 20:5
Hes 14:18
e 1Fa 8:33
Ne 9:2
Eze 6:9
Da 9:5
f Eze 36:31
g Law 26:24
h 1Fa 8:47
2Nya 36:20
i Kum 30:6
Yer 4:4
Mdo 7:51
j Mwa 28:13
k Mwa 26:3
l Mwa 12:7
Kum 4:31
Zb 106:45
m Law 26:34
2Nya 36:20, 21
n 2Fa 17:15
o Kum 4:31
2Fa 13:23
Ne 9:31
p Kum 4:13
Yer 14:21
q Kut 24:3, 8
Kum 9:9
r Eze 20:9

wenu.^a **38** Mtaangamia miongoni mwa mataifa,^b na nchi ya maadui wenu itawala. **39** Wale watakaobaki wataachwa waoze katika nchi za maadui wenu^c kwa sababu ya dhambi zenu. Naam, watao-zea huko kwa sababu ya dhambi za baba zao.^d **40** Kisha wataungama dhambi zao,^e wataungama pia dhambi na ukosefu wa uaminifu wa baba zao, nao watakiri kwamba hawakuwa waaminifu waliponi-pinga mimi.^f **41** Basi nika-lazimika kuwapinga^g kwa kuwapeleka katika nchi ya maadui wao.^h

“Nilifanya hivyo ili mio-yo yao mikaidi* inyenye-kee,ⁱ na ili walipie dhambi zao. **42** Nitakumbuka agano langu na Yakobo,^j na agano langu na Isaka,^k na pia agano langu na Abrahamu,^l nami nitaiku-mbuka nchi yao. **43** Walipo-kuwa wameiacha nchi yao, ilikuwa ikilipa sabato zake^m na kukaa ukiwa bila mtu yeyote, nao walikuwa wakilipia dhambi zao, kwa sababu walika-taa amri zangu na kuchukia sheria zangu.ⁿ **44** Lakini li-cha ya hayo yote, wakiwa ka-tika nchi ya maadui wao, si-tawakataa kabisa^o wala sita-watupa na kuwaangamiza ka-bisa na hivyo kulivungia agano nililofanya^p pamoja nao; kwa maana mimi ni Yehova Mungu wao. **45** Kwa ajili yao nitali-kumbuka agano nililofanya na mababu zao^q niliowatoa nchi-ni Misri mataifa yakishuhud-ia,^r ili nijithibitishe mwenyewe kuwa Mungu wao. Mimi ni Yehova.”

26:41 *Tnn., “mioyo yao ambayo haijatahirwa.”

46 Hayo ndiyo masharti, amri, na sheria ambazo Yehova aliwapa Waisraeli kwenye Mlima Sinai kupitia Musa.^a

27 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Wambie hivi Waisraeli: ‘Mtu akiweka nadhiri ya pekee^b ya kumtolea Yehova thamani inayokadiriwa ya mtu,* **3** thamani ya mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 mpaka miaka 60 itakadiriwa kuwa shekeli 50* za fedha kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.# **4** Lakini ikiwa ni mwanamke, thamani yake itakadiriwa kuwa shekeli 30. **5** Ikiwa mtu ana umri wa kuanzia miaka 5 mpaka miaka 20, thamani ya mwanamume itakadiriwa kuwa shekeli 20 na ya mwanamke shekeli 10. **6** Ikiwa mtu ana umri wa kuanzia mwezi mmoja mpaka miaka mitano, thamani ya mtoto wa kiume itakadiriwa kuwa shekeli tano za fedha na ya mtoto wa kike shekeli tatu za fedha.

7 “Ikiwa mtu ana umri wa miaka 60 na zaidi, thamani ya mwanamume itakadiriwa kuwa shekeli 15 na ya mwanamke shekeli 10. **8** Lakini ikiwa mtu anayeweka nadhiri hawezi kulipa thamani iliyokadiriwa kwa sababu ni maskini sana,^c mtu huyo atasimama mbele ya kuhani, naye kuhani atakadiria thamani yake. Atakadiria thamani yake kulingana na kiasi ambacho mtu anayeweka nadhiri anaweza kulipa.^d

27:2 *Au “nafsi.” 27:3 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. #Au “shekeli takatifu.”

SURA YA 26

a Law 27:34
Kum 6:1

SURA YA 27

b Kum 23:21
Amu 11:30, 31
1Sa 1:11

c Lu 5:7, 11
Law 12:8
Law 14:21

d Lu 21:2-4
2Ko 8:12

Safu ya 2

a Law 20:25
Kum 14:7, 8

b Law 27:19

c Law 27:11, 12

9 “Ikiwa nadhiri inahusi-sha mnyama anayestahili kutolewa kwa Yehova, basi chochote kinachotolewa kwa Yehova kitakuwa kitu kita-katifu. **10** Hawezi kumbadilisha mnyama aliyemweka kuwa nadhiri, yaani, achukue mnyama mzuri na kumtoa mbaya, au achukue mbaya na kumtoa mzuri. Lakini akimbadilisha mnyama huyo na mwingine, wanyama wote wawili watakuwa watakatifu. **11** Ikiwa ni mnyama asiye safi^a ambaye hawezi kutolewa kwa Yehova, mnyama huyo atapelekwa mbele ya kuhani. **12** Halafu kuhani atakadiria thamani yake, ataamua ikiwa ni mzuri au mbaya. Thamani itakayokadiriwa na kuhani ndiyo itakayokuwa thamani ya mnyama huyo. **13** Lakini ikiwa mtu huyo anataka kumnunua tena mnyama huyo, ni lazima alipe thamani ya mnyama huyo pamoja na sehemu ya tano ya thamani iliyokadiriwa.^b

14 “Sasa ikiwa mtu ataitakasa nyumba yake ili iwe takatifu kwa Yehova, kuhani atakadiria thamani ya nyumba hiyo, iwapo ni nzuri au ni mbaya. Thamani itakayokadiriwa na kuhani ndiyo itakayokuwa bei yake.^c **15** Lakini ikiwa mtu anayetakasa nyumba yake anataka kuinunua tena, ni lazima alipe thamani iliyokadiriwa pamoja na sehemu ya tano ya thamani hiyo, kisha itakuwa yake.

16 “Mtu akitakasa sehemu fulani ya shamba lake ili iwe ya Yehova, thamani yake itakadiriwa kulingana na kiasi cha mbegu zinazohitajika

kupandwa: thamani ya homeri moja* ya mbegu za shayiri itakuwa shekeli 50 za fedha. **17** Ikiwa atalitakasa shamba lake kuanzia mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50,^a thamani yake itabaki kama ilivyokadiriwa. **18** Ikiwa atalitakasa shamba lake baada ya mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50, kuhani atakadiria bei kulingana na miaka inayobaki kabla ya mwadhimisho unaofuata wa miaka 50, naye atapunguza thamani iliyokadiriwa.^b **19** Lakini ikiwa yule aliyelitakasa shamba hilo anataka kulinunua tena, ni lazima alipe thamani yake pamoja na sehemu ya tano ya thamani iliyokadiriwa, kisha litakuwa lake. **20** Asipolinunua, kisha mtu mwingine auziwe shamba hilo, haliwezi kununuliwa tena. **21** Yule aliyenunua shamba hilo akiliacha wakati wa Mwadhimisho wa Miaka 50, litakuwa kitu kitakatifu kwa Yehova, shamba lililotolewa kwa ajili yake. Litakuwa mali ya makuhani.^c

22 “Mtu akitakasa shamba alilonunua ambalo si sehemu ya urithi wake na kulitoa liwe mali ya Yehova,^d **23** kuhani amhesabia thamani ya shamba hilo kufikia mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50, na mtu huyo atalipa siku hiyo thamani iliyokadiriwa.^e Ni kitu kitakatifu kwa Yehova. **24** Katika mwaka wa Mwadhimisho wa Miaka 50, shamba litarudishwa kwa yule aliyeliuza, kwa mtu ambaye shamba hilo ni mali yake.^f

27:16 *Homeri ni kipimo sawa na lita 220. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 27

a Law 25:10

b Law 25:15, 16

c Hes 18:8, 14

d Law 25:25

e Law 27:11, 12
Law 27:18

f Law 25:10, 28

Safu ya 2

a Kut 13:2
Hes 18:17b Kut 22:30
Kum 15:19

c Law 27:11-13

d Hes 18:8, 14

e Hes 21:2

f Yos 6:17
1Sa 15:3, 18g Mwa 14:20
Mwa 28:22
Hes 18:21, 26
Kum 14:22
2Nya 31:5
Ne 13:12
Mal 3:10
Lu 11:42
Ebr 7:5

25 “Thamani ya kila kitu itakadiriwa kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu. Shekeli moja ni sawa na gera 20.*

26 “Hata hivyo, hakuna mtu yeyote anayepaswa kumtakasa mzaliwa wa kwanza wa wanyama, kwa sababu mzaliwa wa kwanza ni wa Yehova.^a Awe ni ng’ombe dume au kondoo, tayari ni wa Yehova.^b **27** Ikiwa mtu anamkomboa mnyama asiye safi kulingana na thamani iliyokadiriwa, anapaswa kulipa thamani ya mnyama huyo pamoja na sehemu ya tano ya thamani hiyo.^c Lakini asipomkomboa, mnyama huyo atauzwa kulingana na thamani iliyokadiriwa.

28 “Lakini kitu chochote ambacho mtu anamtolea Yehova bila masharti,* iwe ni mwanadamu au mnyama au shamba lake, hakiwezi kuuza au kununuliwa tena. Kitu chochote kilichowekwa wakfu ni kitakatifu kabisa kwa Yehova.^d **29** Zaidi ya hayo, mtu yeyote aliyehukumiwa na kutengwa ili aangamizwe hawezi kukombolewa.^e Ni lazima auawe.^f

30 “Kila sehemu ya kumi^g ya mazao ya ardhi au matunda ni mali ya Yehova. Sehemu hiyo ni takatifu kwa Yehova. **31** Ikiwa mtu anataka kununua tena sehemu yoyote ya kumi aliyotoa, anapaswa kulipa thamani yake pamoja na sehemu ya tano ya thamani hiyo. **32** Kila sehemu ya kumi ya mifugo na ya

27:25 *Gera moja ilikuwa na uzito wa gramu 0.57. Angalia Nyongeza B14.
27:28 *Au “ili kiangamizwe.”

kundi, yaani, kila mnyama wa kumi anayepita* chini ya fimbo ya mchungaji atakuwa mtakatifu kwa Yehova. **33** Mtu huyo hapaswi kuchunguza ikiwa mnyama huyo ni mzuri au mbaya, wala hapa-

27:32 *Au "kichwa cha kumi kinachopita."

Safu ya 2

SURA YA 27

a Law 27:9,10

b Kut 3:1
Hes 1:1

swi kumbadilisha na mwingine. Ikiwa atambadilisha na mwingine, basi wanyama wote wawili watakuwa watakatifu.^a Hawawezi kununuliwa tena."^a

34 Hizo ndizo sheria ambazo Yehova alimpa Musa kwenye Mlima Sinai ili awape Waisraeli.^b

HESABU

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Wanaume waandikishwa jeshini (1-46)
Walawi hawakuandikishwa jeshini (47-51)
Kambi yapangwa kwa utaratibu (52-54)</p> <p>2 Kambi yapangwa katika makundi ya makabila matatu-matatu (1-34)
Kundi la Yuda upande wa mashariki (3-9)
Kundi la Rubeni upande wa kusini (10-16)
Kambi ya Lawi yawekwa katikati (17)
Kundi la Efraimu upande wa magharibi (18-24)
Kundi la Dani upande wa kaskazini (25-31)
Jumla ya wanaume walioandikishwa (32-34)</p> <p>3 Wana wa Haruni (1-4)
Walawi wachaguliwa ili kuhudumu (5-39)
Kukombolewa kwa wazaliwa wa kwanza (40-51)</p> <p>4 Utumishi wa Wakohathi (1-20)
Utumishi wa Wagershoni (21-28)
Utumishi wa Wamerari (29-33)
Muhtasari kuhusu idadi ya watu waliohesabiwa (34-49)</p> <p>5 Kuwatenga watu wasio safi (1-4)
Kuungama na kulipia kosa (5-10)
Maji yatumiwa kuthibitisha ikiwa mtu alifanya uzinzi (11-31)</p> <p>6 Nadhiri ya Unadhiri (1-21)
Baraka ya makuhani (22-27)</p> <p>7 Matoleo ya kuzindua hema la ibada (1-89)</p> | <p>8 Haruni awasha taa saba (1-4)
Walawi watakaswa na kuanza utumishi wao (5-22)
Mipaka ya umri kwa ajili ya utumishi wa Walawi (23-26)</p> <p>9 Mpango wa kuadhimisha Pasaka baadaye (1-14)
Wingu na moto juu ya hema la ibada (15-23)</p> <p>10 Tarumbeta za fedha (1-10)
Kuondoka Sinai (11-13)
Utaratibu wa kuondoka (14-28)
Hobabu aombwa awaongoze Waisraeli (29-34)
Sala aliyotoa Musa walipokuwa wakianza safari (35, 36)</p> <p>11 Mungu aleta moto kwa sababu ya malalamiko (1-3)
Watu walilia nyama (4-9)
Musa ahisi hastahili (10-15)
Yehova awapa roho wazee 70 (16-25)
Eldadi na Medadi; Yohua aona wivu kwa ajili ya Musa (26-30)
Kware waletwa; watu waadhibiwa kwa sababu ya pupa (31-35)</p> <p>12 Miriamu na Haruni wampinga Musa (1-3)
Musa mtu mpole zaidi kuliko watu wote (3)
Yehova amtetea Musa (4-8)
Miriamu apigwa na ukoma (9-16)</p> <p>13 Wapelelezi 12 watumwa Kanaani (1-24)
Wapelelezi kumi waleta habari mbaya (25-33)</p> |
|--|--|

- 14 Watu wataka kurudi Misri (1-10)
Yoshua na Kalebu waleta habari
nzuri (6-9)
Yehova akasirikia; Musa aingilia
kati (11-19)
Adhabu: miaka 40 nyikani (20-38)
Waisraeli washindwa na
Waamaleki (39-45)
- 15 Sheria kuhusu dhabihu (1-21)
Sheria zilizile kwa wenyeji na
wageni (15, 16)
Dhabihu kwa ajili ya dhambi
zilizofanywa bila kukusudia (22-29)
Adhabu kwa ajili ya dhambi
zilizofanywa kimakusudi (30, 31)
Aliyevunja Sabato auawa (32-36)
Mavazi yawe na upindo wa
nyuzinyuzi (37-41)
- 16 Uasi wa Kora, Dathani, na Abiramu (1-19)
Waasi wahukumiwa (20-50)
- 17 Fimbo ya Haruni iliyochanua maua
yatumika kuwa onyo (1-13)
- 18 Majukumu ya makuhani na Walawi (1-7)
Posho za makuhani (8-19)
Agano la chumvi (19)
Walawi watapokea na kutoa sehemu
moja ya kumi (20-32)
- 19 Ng'ombe mwekundu na maji ya
kutakasa (1-22)
- 20 Miriamu afa kule Kadeshi (1)
Musa aupiga mwamba na hivyo
kutenda dhambi (2-13)
Waedomu wawazuia Waisraeli
kupita (14-21)
Kifo cha Haruni (22-29)
- 21 Mfalme wa Aradi ashindwa (1-3)
Nyoka wa shaba (4-9)
Waisraeli wazunguka Moabu (10-20)
Mfalme Sihoni wa Waamori
ashindwa (21-30)
Mfalme Ogu wa Waamori
ashindwa (31-35)
- 22 Balaki amkodi Balaamu (1-21)
Punda wa Balaamu aongea (22-41)
- 23 Maneno ya kwanza ya kishairi ya
Balaamu (1-12)
Maneno ya pili ya kishairi ya
Balaamu (13-30)
- 24 Maneno ya tatu ya kishairi ya
Balaamu (1-11)
- Maneno ya nne ya kishairi ya
Balaamu (12-25)
- 25 Waisraeli watenda dhambi na
wanawake Wamoabu (1-5)
Finehasi achukua hatua (6-18)
- 26 Makabila ya Waisraeli yahesabiwa
mara ya pili (1-65)
- 27 Mabinti wa Selofehadi (1-11)
Yoshua achaguliwa ili achukue mahali
pa Musa (12-23)
- 28 Taratibu za kutoa dhabihu
mbalimbali (1-31)
Dhabihu ya kila siku (1-8)
Kwa ajili ya Sabato (9, 10)
Dhabihu ya kila mwezi (11-15)
Kwa ajili ya Pasaka (16-25)
Kwa ajili ya Sherehe ya
Majuma (26-31)
- 29 Taratibu za kutoa dhabihu
mbalimbali (1-40)
Siku ya kupiga tarumbeta (1-6)
Siku ya Kufunika Dhambi (7-11)
Sherehe ya Vibanda (12-38)
- 30 Nadhiri za wanaume (1, 2)
Nadhiri za wanawake na
mabinti (3-16)
- 31 Wamidiani walipizwa kisasi (1-12)
Balaamu auawa (8)
Maagizo kuhusu nyara za vita (13-54)
- 32 Waliobaki upande wa mashariki wa
Yordani (1-42)
- 33 Vituo vya safari ya Waisraeli
nyikani (1-49)
Maagizo ya kuteka nchi ya
Kanaani (50-56)
- 34 Mipaka ya Kanaani (1-15)
Wanaume wapewa kazi ya kuigawanya
nchi (16-29)
- 35 Majiji ya Walawi (1-8)
Majiji ya makimbilio (9-34)
- 36 Sheria kuhusu kuwaoa warithi wa
kike (1-13)

1 Na Yehova akazungumza na Musa katika nyika ya Sinai,^a kwenye hema la mku-tano,^b siku ya kwanza ya mwezi wa pili katika mwaka wa pili baada ya Waisraeli kutoka nchini Misri.^c Akamwambia: **2** “Wahesabu^d Waisraeli wote, * kila mmoja wao[#] kulingana na familia yake, kulingana na ukoo wake,^Δ orodhesha majina ya wanaume wote. **3** Wewe na Haruni mnapaswa kuwaandikisha watu wote wenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi^e wanaoweza kutumikia katika jeshi la Israeli, kulingana na vikosi vyao.*

4 “Mchukueni mwanamume mmoja kutoka katika kila kabila, kila mmoja wao anapaswa kuwa kiongozi wa ukoo wake.^{Δf} **5** Haya ndiyo majina ya wanaume watakaowasaidia ninyi: kutoka kabila la Rubeni, Elisuri^g mwana wa Shedeuri; **6** kabila la Simeoni, Shelumieli^h mwana wa Zurishadai; **7** kabila la Yuda, Nashoniⁱ mwana wa Aminadabu; **8** kabila la Isakari, Nethaneli^j mwana wa Zuari; **9** kabila la Zabuloni, Eliabu^k mwana wa Heloni; **10** wana wa Yosefu: kabila la Efraimu,^l Elishama mwana wa Amihudi; kabila la Manase, Gamalieli mwana wa Pedazuri; **11** kabila la Benjamin, Abidani^m mwana wa Gidioni; **12** kabila la Dani, Ahiezeriⁿ mwana wa Amishadai; **13** kabila la Asheri, Pagieli^o mwana wa Okrani; **14** kabila la Gadi, Eliasafu^p mwana wa Deue-

1:2 *Tnn., “wana wote wa Israeli.” #Au “kila kichwa.” 1:2, 4, 18, 20, 22, 24
^ΔYaani, ukoo wa upande wa baba. 1:3
 *Tnn., “kulingana na majeshi yao.”

SURA YA 1

a Kut 19:1
Mdo 7:38

b Kut 25:22

c Kut 40:17

d Kut 30:12

e Kut 30:14

f Kut 18:25
Hes 1:16
Yos 22:13, 14
Yos 23:2
1Nya 27:1

g Hes 2:10

h Hes 7:11, 36

i Ru 4:20
Lu 3:23, 32

j Hes 10:15

k Hes 7:11, 24

l Mwa 48:20

m Hes 2:22

n Hes 7:11, 66

o Hes 7:11, 72

p Hes 2:14
Hes 7:11, 42
Hes 10:20

Safu ya 2

a Hes 2:29
Hes 10:27

b Kut 18:21
Hes 7:2

c Kum 1:15

d Kut 30:14

e Hes 26:1, 2

f Mwa 29:32
Hes 2:10, 11

g Mwa 29:33
Mwa 46:10
Hes 2:12, 13

h Mwa 30:10, 11
Mwa 46:16
Hes 2:14, 15

li; **15** kabila la Naftali, Ahira^a mwana wa Enani. **16** Hao ndio waliochaguliwa miongoni mwa Waisraeli. Hao ndio wakuu^b wa makabila ya baba zao, viongozi wa maelfu katika Israeli.”^c

17 Basi Musa na Haruni wakawachukua wanaume hao waliotajwa majina. **18** Wakawakusanya Waisraeli wote siku ya kwanza ya mwezi wa pili, ili kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi aandikishwe kulingana na jina lake, familia yake, na ukoo wake,^{Δd} **19** kama Yehova alivyomwamuru Musa. Basi akawaandikisha katika nyika ya Sinai.^e

20 Wana wa Rubeni, wazao wa mzaliwa wa kwanza wa Israeli,^f waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.^Δ Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **21** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Rubeni walikuwa 46,500.

22 Wazao wa Simeoni^g waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.^Δ Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **23** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Simeoni walikuwa 59,300.

24 Wazao wa Gadi^h waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.^Δ Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa,

25 wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Gadi walikuwa 45,650.

26 Wazao wa Yuda^a waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **27** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Yuda walikuwa 74,600.

28 Wazao wa Isakari^b waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **29** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Isakari walikuwa 54,400.

30 Wazao wa Zabuloni^c waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **31** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Zabuloni walikuwa 57,400.

32 Wazao wa Yosefu kupitia Efraimu^d waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **33** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Efraimu walikuwa 40,500.

34 Wazao wa Manase^e waliorodheshwa kulingana na

1:26, 28, 30, 32, 34, 36, 38, 40, 42

*Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 1

a Mwa 29:35
Mwa 46:12
Hes 2:3, 4
1Nya 5:2
Mt 1:2
Ebr 7:14

b Mwa 30:17, 18
Mwa 46:13
Hes 2:5, 6

c Mwa 30:20
Hes 2:7, 8

d Mwa 41:51, 52
Mwa 46:20
Mwa 48:17-19
Hes 2:18, 19

e Hes 2:20, 21

Safu ya 2

a Mwa 43:29
Mwa 46:21
Hes 2:22, 23

b Mwa 30:4-6
Mwa 46:23
Hes 2:25, 26
Hes 10:25

c Mwa 35:26
Hes 2:27, 28

d Mwa 30:7, 8
Mwa 46:24
Hes 2:29, 30
Hes 26:48

majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **35** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Manase walikuwa 32,200.

36 Wazao wa Benjamini^a waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **37** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Benjamini walikuwa 35,400.

38 Wazao wa Dani^b waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **39** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Dani walikuwa 62,700.

40 Wazao wa Asheri^c waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **41** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Asheri walikuwa 41,500.

42 Wazao wa Naftali^d waliorodheshwa kulingana na majina yao, familia zao, na ukoo wao.* Kila mwanamume mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambaye angeweza kutumikia katika jeshi alihesabiwa, **43** wale walioandikishwa kutoka katika kabila la Naftali walikuwa 53,400.

44 Hao ndio walioandikishwa na Musa na Haruni na wale wakuu 12 wa Israeli, kila mmoja wao aliwakilisha ukoo wake.* **45** Waisraeli wote wenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi ambao wangeweza kutumikia katika jeshi la Israeli waliandikishwa kulingana na ukoo wao,* **46** watu wote walioandikishwa walikuwa 603,550.^a

47 Lakini Walawi^b hawakuandikishwa pamoja nao, kulingana na makabila ya baba zao.^c **48** Basi Yehova akamwambia Musa: **49** “Ni kabila la Lawi tu ambalo hutaliandikisha, nawe hupaswi kuwahesabu pamoja na Waisraeli wengine.^d **50** Unapaswa kuwaweka rasmi Walawi wasimamie hema la Ushahidi^e na vyombo vyake vyote na kila kitu kilichomo.^f Watabeba hema hilo na vyombo vyake vyote,^g nao watalitunza^h na kupiga kambi kulizunguka.ⁱ **51** Wakati wowote hema hilo linapohamishwa, Walawi ndio wanaopaswa kulifungua;^j na wakati linaposimamishwa, Walawi ndio wanaopaswa kulisimamisha; na mtu yeyote asiye na idhini* akilikaribia anapaswa kuuawa.^k

52 “Kila Mwisraeli anapaswa kupiga hema lake katika kambi aliyogawiwa, kila mwanamume kulingana na kundi lake la makabila matatu,* kulingana na kikosi chake.* **53** Walawi wanapaswa kupiga kambi kuzunguka hema la Ushahidi, ili hasira yangu isi-

1:44, 45; 2:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 1:51 *Tnn., “mgeni yeyote,” yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni. 1:52 *Au “alama yake.” *Tnn., “jeshi lake.”

SURA YA 1

a Mwa 13:16
Mwa 22:17
Mwa 46:3
Kut 38:26
Hes 2:32

b Mwa 29:34
Mwa 46:11
Hes 3:12

c Hes 2:33
Hes 26:63, 64

d Hes 26:62, 63

e Kut 31:18

f Kut 38:21
Hes 3:6, 8

g Hes 4:15
Hes 4:24-26
Hes 4:31-33

h Hes 3:30, 31
Hes 4:12

i Hes 2:17
Hes 3:23, 29
Hes 3:35, 38

j Hes 10:17, 21

k Hes 3:10
Hes 18:22

l Hes 2:2, 34

Safu ya 2

a Hes 8:19
Hes 18:5

b Hes 8:24
Hes 18:2, 3
1Nya 23:32

SURA YA 2

c Hes 1:52

d Hes 7:12
Hes 10:14
Ru 4:20
Mt 1:4

e Hes 1:27

f Hes 7:11, 18
Hes 10:15

g Hes 1:29

h Hes 7:11, 24
Hes 10:16

i Hes 1:31

j Hes 10:14

k Hes 1:20

wawakie Waisraeli;^a na lazima Walawi wawajibike kulitunza* hema la Ushahidi.”^b

54 Waisraeli walifanya mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Musa. Hivyo ndivyo walivyofanya.

2 Yehova akamwambia hivi Musa na Haruni: **2** “Waisraeli wanapaswa kupiga kambi mahali ambapo kundi lao la makabila matatu^c limegawiwa, kila mtu karibu na alama ya ukoo wake.* Wanapaswa kupiga kambi kuelekeana na hema la mkutano, kuzunguka pande zake zote.

3 “Kundi la makabila matatu katika kambi ya Yuda litapiga kambi upande wa mashariki, upande wa mapambazuko ya jua, kulingana na vikosi vyake;* mkuu wa wana wa Yuda ni Nashoni^d mwana wa Aminadabu. **4** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 74,600.^e **5** Kabila la Isakari litapiga kambi kando yake; mkuu wa wana wa Isakari ni Nethaneli^f mwana wa Zuari. **6** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 54,400.^g **7** Kisha kabila la Zabuloni; mkuu wa wana wa Zabuloni ni Eliabu^h mwana wa Heloni. **8** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 57,400.ⁱ

9 “Watu wote walioandikishwa katika majeshi ya kambi ya Yuda ni 186,400. Wanapaswa kuwa wa kwanza kuondoka.^j

10 “Kundi la makabila matatu katika kambi ya Rubeni^k litapiga kambi upande wa kusini, kulingana na vikosi

1:53 *Au “kulilinda; kutumikia katika.” 2:3 *Tnn., “majeshi yake.”

vyake;* mkuu wa wana wa Rubeni ni Elisuri^a mwana wa Shedeuri. **11** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 46,500.^b **12** Kabila la Simeoni litapiga kambi kando yake; mkuu wa wana wa Simeoni ni Shelumieli^c mwana wa Zurishadai. **13** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 59,300.^d **14** Kisha kabila la Gadi; mkuu wa wana wa Gadi ni Eliasafu^e mwana wa Reueli. **15** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 45,650.^f

16 "Watu wote walioandikishwa katika majeshi ya kambi ya Rubeni ni 151,450, nao wanapaswa kuwa wa pili kuondoka.^g

17 "Hema la mkutano lina-pohamishwa,^h kambi ya Walawi inapaswa kuwa katikati ya kambi nyingine zote.

"Wote wanapaswa kusafiri kwa kufuata utaratibu uleule wanaofuata wanapopiga kambi,ⁱ kila mtu mahali pake, kulingana na makundi yao ya makabila matatu-matatu.

18 "Kundi la makabila matatu katika kambi ya Efraimu litapiga kambi upande wa magharibi, kulingana na vikosi vyake;* mkuu wa wana wa Efraimu ni Elishama^j mwana wa Amihudi. **19** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 40,500.^k **20** Kabila la Manase^l litapiga kambi kando yake; mkuu wa wana wa Manase ni Gamalieli^m mwana wa Pedazuri. **21** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 32,200.ⁿ **22** Kisha kabila la Benjamini; mkuu wa wana wa Benjami-

SURA YA 2

a Hes 7:11, 30
Hes 10:18

b Hes 1:21

c Hes 7:11, 36
Hes 10:19

d Hes 1:23

e Hes 7:11, 42
Hes 10:20

f Hes 1:25

g Hes 10:18

h Hes 1:51

i 1Ko 14:33, 40

j Hes 7:11, 48
Hes 10:22

k Hes 1:33

l Mwa 48:20

m Hes 7:11, 54
Hes 10:23

n Hes 1:35

Safu ya 2

a Hes 7:11, 60
Hes 10:24

b Hes 1:37

c Hes 10:22

d Hes 7:11, 66
Hes 10:25

e Hes 1:39

f Hes 7:11, 72
Hes 10:26

g Hes 1:41

h Hes 7:11, 78
Hes 10:27

i Hes 1:43

j Hes 10:25

k Mwa 15:5
Kut 38:26
Hes 1:46
Hes 14:29
Hes 26:51, 64

l Hes 1:47
Hes 26:62, 63

m Hes 3:15

ni ni Abidani^a mwana wa Gideoni. **23** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 35,400.^b

24 "Watu wote walioandikishwa katika majeshi ya kambi ya Efraimu ni 108,100, nao wanapaswa kuwa wa tatu kuondoka.^c

25 "Kundi la makabila matatu katika kambi ya Dani litapiga kambi upande wa kaskazini, kulingana na vikosi vyake;* mkuu wa wana wa Dani ni Ahiezeri^d mwana wa Amishadai. **26** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 62,700.^e **27** Kabila la Asheri litapiga kambi kando yake; mkuu wa wana wa Asheri ni Pagieli^f mwana wa Okrani. **28** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 41,500.^g **29** Kisha kabila la Naftali; mkuu wa wana wa Naftali ni Ahira^h mwana wa Enani. **30** Wale walioandikishwa katika jeshi lake ni watu 53,400.ⁱ

31 "Watu wote walioandikishwa katika majeshi ya kambi ya Dani ni 157,600. Wanapaswa kuwa wa mwisho kuondoka,^j kulingana na kundi lao lenye makabila matatu."

32 Hao ndio Waisraeli walioandikishwa kulingana na koo zao;* watu wote walioandikishwa katika kambi hizo ili kuwa wanajeshi walikuwa 603,550.^k **33** Lakini kama Yehova alivyomwamuru Musa, Walawi hawakuandikishwa^l pamoja na Waisraeli wengine.^m **34** Waisraeli walifanya mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Musa. Hivyo ndivyo walivyopiga kambi kuli-

ngana na makundi yao ya makabila matatu,^a na hivyo ndivyo walivyokuwa wakiondoka,^b kila mmoja kulingana na familia yake na ukoo wake.*

3 Basi hawa ndio waliokuwa wazao wa* Haruni na Musa siku ambayo Yehova alizungumza na Musa kwenye Mlima Sinai.^c **2** Haya ndiyo majina ya wana wa Haruni: Nadabu mzaliwa wa kwanza, Abihu,^d Eleazari,^e na Ithamari.^f **3** Hayo ndiyo majina ya wana wa Haruni waliotiwa mafuta ili watumikie wakiwa makuhani.^g **4** Hata hivyo, Nadabu na Abihu walikufa mbele za Yehova walipomtolea Yehova moto haramu^h katika nyika ya Sinai, nao hawakuwa na wana wowote. Lakini Eleazariⁱ na Ithamari^j waliendelea kutumikia wakiwa makuhani pamoja na Haruni baba yao.

5 Kisha Yehova akamwambia Musa, **6** "Walete watu wa kabila la Lawi^k mbele ya kuhani Haruni ili wamhutumie.^l **7** Watatimiza wajibu wao wa kumtumikia na kuwatumikia Waisraeli wote mbele ya hema la mkutano kwa kufanya kazi za hema la ibada. **8** Watatunza vyombo vyote^m vya hema la mkutano na kutimiza wajibu wao wa kuwatumikia Waisraeli kwa kufanya kazi za hema la ibada.ⁿ **9** Utawakabidhi Walawi kwa Haruni na wanawe. Ni watu waliokabidhiwa, ambao Haruni amekabidhiwa kutoka kati ya Waisraeli.^o **10** Unapaswa kumweka rasmi Haruni na wa-

2:34; 3:15 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 3:1 *Tnn., "hivi ndivyo vilivyokuwa vizazi vya."

SURA YA 2

a Hes 2:2

b Hes 10:28

SURA YA 3

c Kut 19:2

d Law 10:1

1Nya 24:2

e Kut 6:25

Kum 10:6

f Kut 6:23

Kut 38:21

1Nya 6:3

g Kut 28:1

Law 8:2, 3

h Law 10:1, 2

i Hes 3:32

Hes 20:26

j Hes 4:28

Hes 7:8

k Hes 8:6

Hes 18:2

l Hes 1:50

Hes 8:11

m Hes 4:12

n Hes 1:51

o Hes 8:15, 16

Hes 18:6

Safu ya 2

a Kut 40:15

Hes 18:7

b Hes 16:39, 40

1Sa 6:19

2Nya 26:16, 18

c Hes 3:41, 45

d Kut 13:2

Kut 34:19

Hes 18:15

Lu 2:23

e Kut 13:15

f Law 27:26

g Kut 19:1

h Hes 3:39

i Kut 6:16

Hes 26:57

1Nya 23:6

j Kut 6:17

k Kut 6:18

nawe ili watekeleze majukumu yao ya ukuhani,^a na mtu yeyote asiye na idhini* atakayekaribia mahali patakatifu anapaswa kuuawa."^b

11 Yehova akaendelea kumwambia Musa, **12** "Tazama! Mimi nawachukua Walawi kutoka miongoni mwa Waisraeli badala ya wazaliwa wote wa kwanza* wa Waisraeli;^c Walawi watakuwa wangu. **13** Kwa maana kila mzaliwa wa kwanza ni wangu.^d Siku niliyomuua kila mzaliwa wa kwanza katika nchi ya Misri^e nilijitakasia kila mzaliwa wa kwanza katika Israeli kuanzia mzaliwa wa kwanza wa mwanaadamu mpaka wa mnyama.^f Watakuwa wangu. Mimi ni Yehova."

14 Yehova akaendelea kuzungumza na Musa katika nyika ya Sinai,^g akamwambia: **15** "Waandikishe wana wa Lawi kila mmoja kulingana na ukoo wake* na familia yake. Unapaswa kumwandikisha kila mwanamu-me, kuanzia mtoto wa umri wa mwezi mmoja na zaidi."^h **16** Kwa hiyo Musa akawaandikisha kama alivyoagizwa na Yehova, kama alivyoamriwa. **17** Haya ndiyo majina ya wana wa Lawi: Gershoni, Kohathi, na Merari.ⁱ

18 Haya ndiyo majina ya wana wa Gershoni kulingana na familia zao: Libni na Shimeji.^j

19 Wana wa Kohathi kulingana na familia zao walikuwa Amramu, Ishari, Hebroni, na Uzieli.^k

3:10 *Tnn., "mgeni yeyote," yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni. 3:12 *Au "kila kifungu mimba."

20 Wana wa Merari kulingana na familia zao walikuwa Mali^a na Mushi.^b

Hizo ndizo zilizokuwa familia za Walawi kila mmoja kulingana na ukoo wake.*

21 Familia ya Walibni^c na familia ya Washimei zilitokana na Gershoni. Hizo ndizo zilizokuwa familia za Wagershoni. **22** Wanaume wao wote walioandikishwa kuanzia umri wa mwezi mmoja na zaidi walikuwa 7,500.^d **23** Familia za Wagershoni zilipiga kambi nyuma ya hema la ibada^e upande wa magharibi. **24** Mkuu wa ukoo* wa Wagershoni alikuwa Eliasafu mwana wa Laeli. **25** Majukumu ya wana wa Gershoni^f katika hema la mkutano yalikuwa kutunza hema lenyewe pamoja^g na kifuniko chake,^h paziaⁱ la mlango wa hema la mkutano, **26** mapazia ya ua yanayoning'inia,^j pazia la mlango wa ua^k linalozunguka hema la ibada na madhabahu, kamba za hema, na utumishi wote uliohusiana na vitu hivyo.

27 Familia ya Waamramu, familia ya Waishari, familia ya Wahebroni, na familia ya Wauzieli zilitokana na Kohathi. Hizo ndizo zilizokuwa familia za Wakohathi.^l **28** Wanaume wote kuanzia umri wa mwezi mmoja na zaidi walikuwa 8,600; jukumu lao lilikuwa kutunza mahali patakatifu.^m **29** Familia za wana wa Kohathi zilipiga kambi upande wa kusini wa hema la ibada.ⁿ **30** Mkuu wa ukoo* wa familia za Wakohathi alikuwa Elisafani mwana wa Uzieli.^o **31** Ma-

3:20, 24, 30, 35 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 3

a 1Nya 6:29

b Kut 6:19

c 1Nya 6:20

d Hes 4:38-40

e Hes 1:53

f Hes 4:24-26

g Kut 26:7

h Kut 26:14

i Kut 26:36

j Kut 27:9

k Kut 27:16

l Hes 3:19

m Hes 4:34-36

n Hes 1:53

o Kut 6:22
1Nya 6:18

Safu ya 2

a Kut 25:10

b Kut 25:23

c Kut 25:31

d Kut 27:1,2
Kut 30:1-3

e Kut 38:3

f Kut 26:31

g Hes 4:15

h Hes 4:16
Hes 20:28i Hes 3:20
Hes 26:58

j Hes 4:42-44

k Hes 1:53

l Kut 36:20

m Kut 36:31

n Kut 26:32,37
Kut 36:37,38

o Kut 27:19

p Hes 4:31,32

q Kut 27:10,11

r Hes 3:10

jukumu yao yalikuwa kutunza Sanduku la Agano,^a meza,^b kinara cha taa,^c madhabahu,^d vyombo^e vilivyotumiwa katika utumishi wa mahali patakatifu, pazia,^f na utumishi wote uliohusiana na vitu hivyo.^g

32 Kiongozi wa wakuu wa Walawi alikuwa Eleazari^h mwana wa kuhani Haruni, naye aliwasimamia wale waliokuwa na majukumu ya kufanya kazi mahali patakatifu.

33 Familia ya Wamali na familia ya Wamushi zilizotokana na Merari. Hizo ndizo zilizokuwa familia za Merari.ⁱ **34** Wanaume wote walioandikishwa kuanzia umri wa mwezi mmoja na zaidi walikuwa 6,200.^j

35 Mkuu wa ukoo* wa familia za Merari alikuwa Zurieli mwana wa Abihaili. Walipiga kambi upande wa kaskazini wa hema la ibada.^k **36** Wana wa Merari walikuwa na majukumu ya kusimamia viunzi^l vya hema la ibada, fito zake,^m nguzo zake,ⁿ vikalio vyake, vyombo vyake vyote,^o na utumishi wote uliohusiana na vitu hivyo,^p **37** na pia nguzo zote zilizozunguka ua na vikalio vyake,^q vingi vya hema, na kamba za hema hilo.

38 Musa na Haruni na wanaume walipiga kambi mbele ya hema la ibada upande wa mashariki, upande wa mapambazuko ya jua. Walikuwa na wajibu wa kutunza mahali patakatifu kwa niaba ya Waisraeli. Mtu yeyote asiye na idhini* ambaye angekaribia mahali patakatifu angeuawa.^r

39 Wanaume wote Walawi wenye umri wa kuanzia mwe-

3:38 *Tnn., "Mgeni yeyote," yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni.

zi mmoja na zaidi walioandikishwa na Musa na Haruni kulingana na familia zao, kama Yehova alivyoagiza, walikuwa 22,000.

40 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Waandikishe wazaliwa wote wa kwanza wa kiume wa Waisraeli kuanzia umri wa mwezi mmoja na zaidi,^a wahesabu na kuorodhesha majina yao. **41** Wachukue Walawi kwa ajili yangu badala ya wazaliwa wote wa kwanza wa Waisraeli,^b mimi ni Yehova, chukua pia mifugo ya Walawi badala ya wazaliwa wote wa kwanza wa mifugo ya Waisraeli.”^c **42** Ndipo Musa akawaandikisha wazaliwa wote wa kwanza wa Waisraeli kama Yehova alivyomwamuru. **43** Wazaliwa wote wa kwanza wa kiume walioandikishwa kwa majina kuanzia umri wa mwezi mmoja na zaidi walikuwa 22,273.

44 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **45** “Wachukue Walawi badala ya wazaliwa wote wa kwanza wa Waisraeli, chukua pia mifugo ya Walawi badala ya mifugo ya Waisraeli, na Walawi watakuwa wangu. Mimi ni Yehova. **46** Ili kulipia bei ya fidia^d ya wale wazaliwa wa kwanza 273 wa Waisraeli ambao wanazidi idadi ya Walawi,^e **47** chukua shekeli tano* kwa ajili ya kila mmoja wao,^f kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.^g Shekeli moja ni sawa na gera 20.^{ag} **48** Utaimpa Haruni na wanawe pesa

3:47 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. ^aAu “shekeli takatifu.” ^gGera moja ilikuwa na uzito wa gramu 0.57. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 3

a Hes 3:15

b Hes 3:12

c Kut 13:2
Hes 18:15

d Hes 18:15

e Hes 3:39, 43

f Hes 18:15, 16

g Law 27:25

Safu ya 2

SURA YA 4

a Hes 3:19, 27

b 1Nya 23:3
Lu 3:23

c Hes 8:25, 26

d Hes 4:30
1Nya 6:48e Hes 3:30, 31
Hes 4:15f Kut 26:31
Kut 40:3
Law 16:2

g Kut 25:10

h Kut 25:13

i Kut 25:23, 24

j Kut 25:29

hizo ambazo ni bei ya fidia ya wale wanaozidi idadi yao.”

49 Kwa hiyo Musa akachukua pesa za ukombozi kutoka kwa wale waliozidi idadi ya wale waliofidiwa na Walawi. **50** Alichukua pesa hizo kutoka kwa wazaliwa wa kwanza wa Waisraeli, shekeli 1,365, kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu. **51** Kisha Musa akampa Haruni na wanawe pesa hizo za fidia kulingana na neno la* Yehova, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

4 Yehova akamwambia hivi Musa na Haruni: **2** “Mnapaswa kuwahesabu wana wa Kohathi^a miongoni mwa wana wa Lawi, kulingana na familia zao na koo zao,* **3** wote wenye umri wa miaka 30^b hadi 50^c walio katika kikundi kilichogawiwa kutumikia katika hema la mkutano.^d

4 “Huu ndio utumishi wa wana wa Kohathi katika hema la mkutano.^e Unahusiana na vitu vitakatifu kabisa: **5** Wakati wa kuvunja kambi, Haruni na wanawe wataingia na kulishusha pazia linaloning’inia mbele ya sanduku la Ushahidi^f na kulifunika kwa pazia hilo.^g **6** Wataweka kifuniko cha ngozi ya sili juu yake na kutandaza juu yake kitambaa cha bluu, halafu wataingiza fito za kubebea^h sanduku hilo.

7 “Pia watafunika meza ya mikate ya wonyeshoⁱ kwa kitambaa cha bluu, na juu yake wataweka sahani, vikombe, mabakuli, na magudulia ya toleo la kinywaji;^j mikate ya

3:51 *Tnn., “kinywa cha.” 4:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

wonyesho ambayo huwa juu ya meza hiyo daima^a inapaswa kubaki juu yake. **8** Watafunika vitu hivyo kwa kitambaa chekundu na juu yake wataweka kifuniko cha ngozi ya sili na kuingiza fito za kuibeba.^b **9** Kisha watachukua kitambaa cha bluu na kukifunika kinara cha taa^c pamoja na taa zake,^d koleo zake, vye-tezo vyake,^e na vyombo vyake vyote vya kuwekea mafuta. **10** Nao wataweka kinara hicho pamoja na vyombo vyake vyote ndani ya ngozi ya sili na kukiweka juu ya ufito wa kubebea. **11** Kisha watatandaza kitambaa cha bluu juu ya madhabahu ya dhahabu^f na kuifunika kwa kifuniko cha ngozi ya sili, halafu wataingiza fito za kuibeba.^g **12** Nao watachukua vyombo vyote^h wanavyotumia kwa ukawaida wanapohudumu mahali patakatifu na kuviweka ndani ya kitambaa cha bluu na kuvifunika kwa kifuniko cha ngozi ya sili, kisha wataviweka juu ya ufito wa kubebea.

13 "Wataondoa majivu* yaliyo kwenye madhabahuⁱ na kutandaza kitambaa cha sufu cha zambarau juu ya madhabahu hiyo. **14** Kisha wataweka juu yake vyombo vyake vyote wanavyotumia kuhudumu kwenye madhabahu: vyetemu, nyuma,* sepetu, na mabakuli, vyombo vyote vya madhabahu;^j watatandaza juu yake kifuniko cha ngozi ya sili na kuingiza fito za kuibeba.^k

15 "Ni lazima Haruni na wanawe wamalize kufunika mahali patakatifu^l na vyombo

4:13 *Au "majivu yenye mafuta," yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhahabu.

4:14 *Wingi wa kifaa kinachoitwa uma.

SURA YA 4

a Law 24:5, 6

b Kut 25:28

c Kut 25:31

d Kut 25:37

e Kut 25:38

f Kut 30:1
Kut 37:25, 26

g Kut 30:5

h Hes 3:30, 31

i Law 6:12

j Kut 27:3

k Kut 27:6

l Hes 4:5

Safu ya 2

a Hes 7:6-9
1Nya 15:2

b 2Sa 6:6, 7

c Hes 3:32

d Kut 27:20

e Kut 30:34, 35

f Kut 30:23-25

g Hes 3:27

h Hes 4:4

i Kut 19:21
1Sa 6:19

j Hes 3:21

vyote vya mahali patakatifu kabla ya watu kuanza safari. Kisha wana wa Kohathi watakuja kuvibeba,^a lakini hawapaswi kugusa vitu vitakatifu, la sivyo watakufa.^b Wana wa Kohathi ndio walio na jukumu la kubeba vitu vya hema la mkutano.

16 "Eleazari^c mwana wa kuhani Haruni ana jukumu la kusimamia mafuta kwa ajili ya taa,^d uvumba uliotiwa manukato,^e toleo la kawaida la nafaka, na mafuta yanayotumiwa kutia mafuta.^f Ndiye anayesimamia hema lote la ibada na vitu vyote vilivyomo, pamoja na mahali patakatifu na vyombo vyake."

17 Yehova akaendelea kuwambia Musa na Haruni: **18** "Msiache familia za Wakohathi^g ziangamizwe kutoka miongoni mwa Walawi. **19** Lakini fanyeni jambo hili ili waendeleo kuishi nao wasife kwa sababu ya kukaribia vitu vitakatifu kabisa.^h Haruni na wanawe wataingia humo na kungawia kila mmoja wao kazi yake na vitu anavyopaswa kubeba. **20** Hawapaswi kuingia hemani na kuona vitu vitakatifu hata kwa muda mfupi, la sivyo watakufa."ⁱ

21 Kisha Yehova akamwambia Musa: **22** "Wana wa Gershoni^j wanapaswa kuhesabiwa kulingana na koo zao* na familia zao. **23** Utawaandikisha wanaume wote wenyewe umri wa miaka 30 hadi 50 walio katika kikundi kilichogawiwa kutumikia katika hema la mkutano. **24** Huu ndio utumishi ambao watu wa familia za Wagershoni wame-

4:22 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

gawiwa kufanya na vitu wana-
vyopaswa kubeba:^a **25** Wata-
beba vitambaa vya hema
la ibada,^b hema la mkuta-
no, kifuniko chake na kifun-
iko cha ngozi ya sili kilicho
juu yake,^c pazia la mlango wa
hema la mkutano,^d **26** mapaz-
ia ya ua yanaying'inia,^e paz-
ia la mlango wa ua^f unaozu-
nguka hema la ibada na ma-
dhabahu, kamba za hema hilo
na vyombo vyake vyote, na
vitu vyote vinavyotumiwa ka-
tika utumishi wa hema la iba-
da. Hiyo ndiyo kazi waliyo-
gawiwa. **27** Haruni na wana-
we watasimamia utumishi
wote wa Wagershoni^g pamoja
na vitu wanavyopaswa kuba-
ba; utawapa jukumu la kuba-
ba vitu hivyo vyote. **28** Huo
ndio utumishi utakaofanywa
na familia za Wagershoni ka-
tika hema la mkutano,^h wata-
simamiwa na Ithamariⁱ mwa-
na wa kuhani Haruni.

29 "Utawaandikisha wana
wa Merari^j kulingana na fa-
milia zao na ukoo wao.*
30 Utawaandikisha wote we-
nye umri wa miaka 30 hadi
50 walio katika kikundi kili-
chogawiwa kutumikia katika
hema la mkutano. **31** Ni ju-
kumu lao kubeba^k vitu vifuata-
vyo vinavyohusiana na utumi-
shi wao katika hema la mkuta-
no: viunzi^l vya hema la ibada,
fito zake,^m nguzo zake,ⁿ vika-
lio vyake;^o **32** nguzo^p za ua
unaozunguka pande zote, vi-
kalio vyake,^q vingi vyake vya
hema,^r na kamba za hema hilo
pamoja na vifaa vyake vyote
na utumishi wote unaohusiana
na hema la ibada. Utamgawia

4:29, 34, 38, 40, 42 *Yaani, ukoo wa
upande wa baba.

SURA YA 4

a Hes 3:25, 26

b Kut 26:1

c Kut 26:7, 14

d Kut 26:36

e Kut 27:9

f Kut 27:16

g Hes 3:21, 23

h Hes 3:25, 26

i Kut 6:23

Hes 4:33

Hes 7:8

j Kut 6:19

Hes 3:33

k Hes 3:36, 37

l Kut 26:15

m Kut 26:26

n Kut 26:37

Kut 36:38

o Kut 26:19

Kut 38:27

p Kut 27:10

q Kut 27:11

r Kut 27:19

Safu ya 2

a Hes 3:33

b Hes 4:28

c Hes 1:16

d Hes 3:19, 27

e Hes 4:47

Hes 8:25, 26

f Hes 3:27, 28

g Hes 3:15

h Hes 3:21

i Hes 3:21, 22

j Hes 4:22, 23

k Hes 8:25, 26

kila mmoja wao kwa jina vifaa
anavyopaswa kubeba. **33** Hi-
vyo ndivyo familia za wana wa
Merari^a zitakavyotumikia kati-
ka hema la mkutano chini ya
usimamizi wa Ithamari mwana
wa kuhani Haruni.^b

34 Kisha Musa na Haruni
na wakuu^c wa Israeli waka-
waandikisha wana wa Koha-
thi^d kulingana na familia zao
na ukoo wao,* **35** wote we-
nye umri wa miaka 30 hadi
50 walio katika kikundi kili-
chogawiwa kutumikia katika
hema la mkutano.^e **36** Wote
walianandikishwa kulingana na
familia zao walikuwa 2,750.^f

37 Hao ndio walianandiki-
shwa kutoka katika familia
za Wakohathi, wote walitumi-
kia katika hema la mkutano.
Musa na Haruni waliwaandiki-
sha kama Yehova alivyoagiza
kupitia Musa.^g

38 Wana wa Gershoni^h wa-
liandikishwa kulingana na fa-
milia zao na ukoo wao,*
39 wote wenye umri wa mia-
ka 30 hadi 50 walio katika ki-
kundi kilichogawiwa kutumi-
kia katika hema la mkutano.

40 Wote walianandikishwa ku-
lingana na familia zao na
ukoo wao* walikuwa 2,630.ⁱ

41 Hao ndio walianandikishwa
kutoka katika familia za wana
wa Gershoni, wote walitumi-
kia katika hema la mkutano.
Musa na Haruni waliwaandiki-
sha kama Yehova alivyoagiza.^j

42 Wana wa Merari walian-
dikishwa kulingana na fa-
milia zao na ukoo wao,*

43 wote wenye umri wa
miaka 30 hadi 50 walio kati-
ka kikundi kilichogawiwa ku-
tumikia katika hema la mku-
tano.^k **44** Wote walianandiki-
shwa kulingana na familia

zao walikuwa 3,200.^a **45** Hao ndio walioandikishwa kuto-ka katika familia za wana wa Merari, ambao waliandikishwa na Musa na Haruni kama Yehova alivyoagiza kupitia Musa.^b

46 Musa na Haruni na wakuu wa Israeli waliwaandikisha Walawi hao wote kulingana na familia zao na koo zao;*

47 walikuwa na umri wa miaka 30 hadi miaka 50, na wote waligawiwa kazi ya kutumikia katika hema la mkutano na kubeba mizigo ya hema hilo.^c

48 Wote walioandikishwa walikuwa 8,580.^d **49** Waliandikishwa kama Yehova alivyoagiza kupitia Musa, kila mmoja wao kulingana na utumishi wake na mzigo aliopaswa kubeba; waliandikishwa kama Yehova alivyomwamuru Musa.

5 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Waanamuru Waisraeli wamtoe nje ya kambi kila mtu mwenye ukoma^e na kila mtu anayetokwa na umajimaji^f na kila mtu aliyejichafua kwa kumgusa mtu aliyekufa.*^g **3** Mnapaswa kumtoa nje awe ni mwanamume au mwanamke. Mnapaswa kuwatoa nje ya kambi watu hao ili wasichafue^h kambi za wale ninaokaa* kati yao.”ⁱ **4** Basi Waisraeli wakafanya hivyo, wakawatoa nje ya kambi. Waisraeli wakafanya kama Yehova alivyomwambia Musa.

5 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **6** “Waambie Waisraeli, ‘Mwanamume au mwanamke akitenda dhambi yoyote ya kibinadamu na ku-

4:46 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. **5:2** *Au “kugusa nafsi iliyokufa.” Angalia Kamusi, uku. 2012. **5:3** *Au “ninao-piga hema.”

SURA YA 4

a Hes 3:33, 34

b Hes 4:29

c Hes 4:15
Hes 4:24-26
Hes 4:31-33

d Hes 3:39

SURA YA 5

e Law 13:45, 46

f Law 15:2

g Law 22:4
Hes 19:11

h Hes 19:22

i Kut 25:8
Law 26:11

Safu ya 2

a Law 5:1, 17

b Law 5:5
Yos 7:19
Yak 5:16

c Law 6:4, 5

d Law 5:16
Law 6:6, 7
Law 7:7e Law 6:14, 17
Law 7:1, 6
Law 10:12, 13f Kut 29:27, 28
Hes 18:8
Kum 18:3
Eze 44:29
1Ko 9:13g Law 18:20
Kum 5:18

kosa kuwa mwaminifu kwa Yehova, mtu huyo ana* hatia.^a

7 Ni lazima aungame^b dhambi aliyotenda na alipe malipo kamili kwa ajili ya hatia yake na kuongeza sehemu ya tano ya malipo hayo;^c atampa yule aliyemkosea. **8** Lakini ikiwa mtu aliyekosewa hana mtu wa karibu wa ukoo atakayepokea malipo hayo, yanapaswa kurudishwa kwa Yehova nayo yatakuwa ya kuhani, isipokuwa kondoo dume wa dhabihu ya kufunika dhambi atakayetolewa kufunika dhambi yake.^d

9 “Kila mchango mtakatifu^e kutoka kwa Waisraeli unaoletwa kwa kuhani utakuwa wake.^f **10** Vitu vitakatifu vya kila mtu vitaendelea kuwa vyake mwenyewe. Kitu chochote ambacho mtu anampa kuhani kitakuwa cha kuhani.”

11 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **12** “Waanamie Waisraeli, ‘Hivi ndivyo mtakavyofanya mke wa mtu yeyote akipotoka na kukosa uaminifu kwa mume wake **13** na mwanamume mwingine afanye naye ngono,^g lakini mume wake hajui jambo hilo na halijagunduliwa, kwa hiyo mwanamke huyo amejichafua lakini hakuna shahidi wa kumshtaki, naye hajakamatwa: **14** Iwe mume wake ana wivu na anatilia shaka uaminifu wa mke wake aliyejichafua, au iwe ana wivu na anatilia shaka uaminifu wa mke wake ingawa hajajichafua, **15** ni lazima mwanamume huyo ampeleke mke wake kwa kuhani pamoja na toleo kwa ajili yake, yaani, sehemu ya kumi ya ki-

5:6 *Au “nafsi hiyo ina.”

pimo cha efa* ya unga wa shayiri. Hapaswi kumimina mafuta juu ya toleo hilo wala kutia ubani juu yake, kwa sababu ni toleo la nafaka la wivu, toleo la nafaka ambalo ni kumbukumbu la hatia.

16 “Kuhani atamleta mwanamke huyo na kumsimamisha mbele za Yehova.^a **17** Kisha kuhani atatia maji matakatifu katika chombo cha udongo na kuchukua kiasi kidogo cha mavumbi kutoka kwenye sakafu ya hema la ibada na kuyatia katika maji hayo. **18** Baada ya kuhani kumsimamisha mwanamke huyo mbele za Yehova, atafungua nywele za mwanamke huyo na kuweka katika mikono ya mwanamke huyo lile toleo la nafaka la kumbukumbu, yaani, toleo la nafaka la wivu,^b huku kuhani akiwa ameshika mkononi yale maji machungu yanayoleta laana.^c

19 “Kisha kuhani atamwapisha mwanamke huyo akisema: “Ikiwa hujafanya ngono na mwanamume mwingine ukiwa chini ya mamlaka ya mume wako^d wala hujapotoka au kujichafua, basi maji haya machungu yanayoleta laana yasikudhuru. **20** Lakinikiwa umepotoka ukiwa chini ya mamlaka ya mume wako na kujichafua kwa kufanya ngono na mwanamume mwingine^e ambaye si mume wako—” **21** Basi kuhani atamwapisha mwanamke huyo kiapo chenye laana, na kumwambia: “Yehova na akufanye uwe mfano wa laana na kiapo miongoni mwa watu

5:15 *Sehemu ya kumi ya efa ilikuwa sawa na lita 2.2 au kilogramu 1.3 hivi. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 5

a Yer 17:10
Ebr 13:4

b Hes 5:15, 25

c Hes 5:22, 24

d Ro 7:2

e Law 18:20
1Ko 6:9,10

Safu ya 2

a Hes 5:15

b Law 2:9

wako, Yehova na akufanye uwe tasa* na tumbo lako livimbe. **22** Maji haya yanayoleta laana yataingia katika matumbo yako na kufanya tumbo lako livimbe nawe utakuwa tasa.”* Kisha mwanamke huyo atasema: “Amina! Amina!”[#]

23 “Halafu kuhani ataandika laana hizo katika kitabu na kuziosha kwenye maji machungu ili zifutike. **24** Kisha atamnyweshwa mwanamke huyo maji hayo machungu yanayoleta laana, na maji hayo yanayoleta laana yataingia mwilini mwake na kusababisha maumivu makali. **25** Kuhani atachukua toleo la nafaka la wivu^a kutoka mkononi mwa mwanamke huyo na kulitikisa kwenda mbele na nyuma mbele za Yehova, kisha atalileta karibu na madhabahu. **26** Halafu kuhani atachukua mkono mmoja wa toleo la nafaka ili kuwa dhahihu ya kumbukumbu na kulateketeza juu ya madhabahu ili lifuke moshi,^b kisha atamnyweshwa mwanamke huyo maji hayo. **27** Baada ya mwanamke huyo kunyweshwa maji hayo, ikiwa amejichafua na kukosa uaminifu kwa mume wake, maji yanayoleta laana yataingia mwilini mwake na kusababisha maumivu makali, na tumbo lake litavimba naye atakuwa tasa,* na mwanamke huyo atakuwa

5:21 *Tnn., “afanye paja lako lidhoofike.” Inaonekana msemu huu unarejelea viungo vya uzazi. 5:22 *Tnn., “na paja lako litadhoofika.” Inaonekana msemu huu unarejelea viungo vya uzazi. #Au “Na iwe hivyo! Na iwe hivyo!” 5:27 *Tnn., “na paja lake litadhoofika.” Inaonekana msemu huu unarejelea viungo vya uzazi.

mfano wa laana miongoni mwa watu wake. **28** Hata hivyo, ikiwa mwanamke huyo hajajichafua, naye ni safi, basi hatapata madhara, ata-weza kupata mimba na kuzaa watoto.

29 “Hiyo ndiyo sheria kuhusu wivu^a inayopaswa kufuatwa mwanamke akipotoka na kujichafua akiwa chini ya mamlaka ya mume wake, **30** au ikiwa mwanamume ana wivu na anatilia shaka uaminifu wa mke wake; mwanamume huyo atamsimamisha mke wake mbele za Yehova, naye kuhani atamtendea mwanamke huyo kulingana na sheria hii yote. **31** Mwanamume huyo hatakuwa na hatia, lakini mke wake ataadhibiwa kwa sababu ya kosa lake.”

6 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Wambie hivi Waisraeli: ‘Mwanamume au mwanamke akiweka nadhiri ya pekee ya kuishi akiwa Mnadhiri*^b kwa Yehova, **3** anapaswa kujiepusha na divai na vinywaji vingine vyenye kileo. Hapaswi kunywa siki ya divai au siki ya kitu chochote chenye kileo.^c Hapaswi kamwe kunywa maji ya zabibu, wala kula zabibu zilizotoka kuchumwa au zilizokau-shwa. **4** Siku zote atakazokuwa Mnadhiri hapaswi kula kitu chochote kinachotokana na mzabibu, kuanzia zabibu ambazo hazijaiva mpaka maganda yake.

5 “Siku zote atakazokuwa Mnadhiri hakuna wembe utakaogusa kichwa chake.^d Atae-

6:2 *Katika Kiebrania ni *na-zir'*, lina-lomaanisha “Aliyetengwa; Aliyewekwa Wakfu; Aliyewekwa Kando.”

SURA YA 5

^a Hes 5:14, 15

SURA YA 6

^b Amu 13:5

^c Law 10:9
Amo 2:11, 12
Lu 1:15

^d Amu 13:5
Amu 16:17
1Sa 1:11

Safu ya 2

^a Law 21:1, 11

^b Hes 19:14

^c Hes 6:13, 18

^d Law 5:8, 10

ndelea kuwa mtakatifu kwa kuacha nywele za kichwa chake ziwe ndefu mpaka siku alizojitenga kwa ajili ya Yehova zitakapokwisha. **6** Siku zote alizojitenga kwa ajili ya Yehova hapaswi kumkaribia mtu aliyekufa.* **7** Hata baba yake au mama yake au ndugu yake au dada yake akifa, hapaswi kujichafua,^a kwa sababu ishara ya kwamba yeye ni Mnadhiri kwa Mungu iko juu ya kichwa chake.

8 “Atakuwa mtakatifu kwa Yehova siku zote atakazokuwa Mnadhiri. **9** Lakini mtu akifa ghafla kando yake^b na kuchafua nywele zake ambazo ni ishara ya kwamba amejitenga kwa ajili ya Mungu,* ni lazima anyoe kichwa chake^c siku anapothibitisha utakaso wake. Anapaswa kukinyoa siku ya saba. **10** Na siku ya nane anapaswa kumpelekea kuhani njiwa tetere wawili au hua wawili wachanga kwenye mlango wa hema la mkutano. **11** Kuhani atamtoa ndege mmoja kuwa dhabihu ya dhambi na mwingine kuwa dhabihu ya kuteketewa ili kufunika dhambi aliyotenda^d kwa kumgusa mtu aliyekufa.* Kisha anapaswa kutakasa kichwa chake siku hiyo. **12** Ni lazima ajitenge tena kwa ajili ya Yehova na kuanza upya siku za Unadhiri wake, naye ataleta mwanakondoo dume wa mwaka mmoja kuwa dhabihu ya hatia. Hata hivyo, zile siku za awali hazitahesa-

6:6 *Au “kuikaribia nafsi iliyokufa.” Angalia Kamusi, uku. **6:9** *Au “kutia unajisi kichwa cha Unadhiri wake.” **6:11** *Au “kugusa nafsi iliyokufa.”

biwa kwa sababu aliuchafua Unadhiri wake.

13 “Hii ndiyo sheria inayomhusu Mnadhiri: Atakapomaliza siku zake za kuwa Mnadhiri,^a ataletwa kwenye mlango wa hema la mkutano.

14 Akiwa hapo atamtolea Yehova dhabihu zake: mwanakondoo dume wa mwaka mmoja asiye na kasoro kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa,^b mwanakondoo jike wa mwaka mmoja asiye na kasoro kwa ajili ya dhabihu ya dhambi,^c kondoo dume mmoja asiye na kasoro kwa ajili ya dhabihu ya ushirika,^d **15** kikapu cha mikate ya mvingingo isiyo na chachu na iliyokwa kwa unga laini uliochanganywa na mafuta, mikate myembamba isiyo na chachu na iliyopakwa mafuta, na toleo la nafaka^e na matoleo ya vinywaji ya dhabihu hizo.^f **16** Kuhani atatoa vitu hivyo mbele za Yehova na kutoa dhabihu ya dhambi na dhabihu ya kuteketezwa kwa ajili ya mtu huyo. **17** Kisha atamtolea Yehova kondoo dume kwa ajili ya dhabihu ya ushirika pamoja na kikapu cha mikate isiyo na chachu, pia atatoa toleo la nafaka^g pamoja na toleo la kinywaji la dhabihu huyo.

18 “Halafu ni lazima Mnadhiri huyo anyoe nywele za kichwa chake^{*h} kwenye mlango wa hema la mkutano, naye atachukua nywele hizo za Unadhiri wake na kuzitia katika moto ulio chini ya dhabihu ya ushirika. **19** Kisha kuhani atachukua mguu wa mbele uliochemshwaⁱ wa yule kondoo dume, mkate mmoja wa

6:18 *Au “kichwa cha Unadhiri wake.”

SURA YA 6

a Hes 30:2
Mhu 5:4

b Law 1:10

c Law 4:32

d Law 3:1

e Law 2:1
Law 6:14

f Hes 15:8, 10

g Law 2:9

h Hes 6:5

i Law 8:31

Safu ya 2

a Kut 29:23, 24

b Law 7:34

c Amu 13:5

d Law 9:22
Kum 10:8

e Ru 2:4
Zb 134:3

f Zb 31:16
Zb 67:1

g Zb 29:11
Lu 2:14

h Kum 28:10
Isa 43:7, 10

i Zb 5:12
Zb 67:7

SURA YA 7

j Kut 40:17

k Kut 30:26

l Law 8:10

m Kut 40:10

mvingingo usio na chachu kutoa katika kile kikapu, na mka-te mmoja mwembamba usio na chachu, na kuviweka mikononi mwa Mnadhiri huyo baada ya nywele zake za Unadhiri kunyolewa. **20** Halafu kuhani atavitikisa vitu hivyo kwenda mbele na nyuma vi-kiwa toleo la kutikiswa mbele za Yehova.^a Ni vitu vitakati-fu kwa kuhani, pamoja na ki-dari cha toleo la kutikiswa na mguu uliotolewa kama mchango.^b Baada ya hayo, Mnadhiri huyo anaweza kunywa divai.

21 “Hii ndiyo sheria inayomhusu Mnadhiri^c anayeweka nadhiri: Akiweka nadhiri na iwe kwamba anaweza kumtolea Yehova toleo ambalo hali-hitajiwi katika kutimiza Unadhiri wake, ni lazima atimize nadhiri yake kulingana na sheria ya Unadhiri wake.”

22 Kisha Yehova akamwambia Musa: **23** “Mwambie hivi Haruni na wanawe: ‘Hivi ndivyo mtakavyowabariki^d Waisraeli. Waambieni:

24 “Yehova na awabariki^e na kuwalinda.

25 Yehova na awangazie nuru ya uso wake,^f na kuwapa kibali chake.

26 Yehova na ainue uso wake kuwaelekea na kuwapa amani.”^g

27 Ni lazima waliweke jina langu juu ya Waisraeli,^h ili niwabariki Waisraeli.”ⁱ

7 Siku ambayo Musa alimaliza kutengeneza hema la ibada,^j alilitia mafuta^k na kulitakasa pamoja na vyombo vyake vyote, na madhabahu na vyombo vyake vyote.^l Baada ya kuvitia mafuta na kuvitakasa vitu hivyo,^m **2** wakuu

wa Israeli,^a viongozi wa koo zao,* wakaleta matoleo. Wakuu hao wa makabila waliosimamia kazi ya kuwaandikisha watu **3** wakamletea Yehova matoleo yao; walileta magari sita yaliyofunikwa na pia ng'ombe dume 12, gari moja kutoka kwa kila wakuu wawili na ng'ombe dume mmoja kutoka kwa kila mkuu; wakaleta vitu hivyo mbele ya hema la ibada. **4** Yehova akamwambia Musa: **5** "Pokea vitu hivyo kutoka kwao, kwa maana vitatumiwa katika utumishi wa hema la mkutano, nawe unapaswa kuwapa Walawi vitu hivyo, utampa kila mmoja kulingana na mahitaji ya kazi yake."

6 Basi Musa akapokea magari hayo pamoja na ng'ombe na kuwapa Walawi. **7** Aliwapa wana wa Gershoni magari mawili na ng'ombe dume wanne kulingana na mahitaji ya kazi yao;^b **8** akawapa wana wa Merari magari manne na ng'ombe dume wanane kulingana na mahitaji ya kazi yao, chini ya usimamizi wa Ithamari mwana wa kuhani Haruni.^c **9** Lakini hakuwapa chochote wana wa Kohathi kwa sababu majukumu yao yalihusisha kutumikia mahali patakatifu,^d nao walibeba vitu vitakatifu mabegani.^e

10 Basi wakuu wakaleta matoleo yao siku ya kuizindua^f madhabahu na kutia mafuta. Wakuu walipoleta matoleo yao mbele ya madhabahu, **11** Yehova akamwambia Musa: "Kila siku, mkuu mmoja ataleta matoleo yake kwa ajili ya kuizindua madhabahu."

7:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.
7:10 *Au "kuweka wakfu."

SURA YA 7

a Kut 18:21
Hes 1:4, 16

b Hes 3:25, 26
Hes 4:24-26

c Hes 3:36, 37
Hes 4:31-33

d Hes 3:30, 31
Hes 4:15

e 2Sa 6:13
1Nya 15:15

f 1Fa 8:63
2Nya 7:5

Safu ya 2

a Hes 1:4, 7
Hes 2:3
Ru 4:20
Mt 1:4

b Law 27:25

c Law 2:1

d Law 1:3

e Law 4:22, 23

f Law 3:1

g Kut 6:23
Lu 3:23, 33

h Hes 1:4, 8
Hes 2:5
Hes 10:15

i Law 27:25

12 Yule aliyelea matoleo yake siku ya kwanza alikuwa Nashoni^a mwana wa Aminadabu wa kabila la Yuda. **13** Alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130* na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^{#b} vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^c **14** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba;* **15** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketewa;^d **16** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^e **17** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^f alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Nashoni mwana wa Aminadabu.^g

18 Siku ya pili, Nethaneli^h mwana wa Zuari, mkuu wa Isakari, alileta matoleo yake. **19** Alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,ⁱ vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili

7:13 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.
#Au "shekeli takatifu." 7:14 *Au "bakuli dogo lenye uzito wa shekeli 10, lililojaa uvumba."

ya toleo la nafaka;^a **20** kiko-mbe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichoja uvumba; **21** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwana-kondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^b **22** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^c **23** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^d alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Nethaneli mwana wa Zuari.

24 Siku ya tatu, mkuu wa wana wa Zabuloni, Eliabu^e mwana wa Heloni, **25** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^f vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^g **26** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichoja uvumba; **27** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^h **28** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;ⁱ **29** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^j alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwa-

SURA YA 7

a Law 2:1

b Law 1:3

c Law 4:22, 23

d Law 3:1

e Hes 2:7
Hes 10:16

f Law 27:25

g Law 2:1

h Law 1:3

i Law 4:22, 23

j Law 3:1

Safu ya 2

a Hes 1:4, 9

b Hes 2:10
Hes 10:18

c Law 27:25

d Law 2:1

e Law 1:3

f Law 4:22, 23

g Law 3:1

h Hes 1:4, 5

i Hes 2:12

j Law 27:25

k Law 2:1

ka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Eliabu^a mwana wa Heloni.

30 Siku ya nne, mkuu wa wana wa Rubeni, Elisuri^b mwana wa Shedeuri, **31** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^c vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^d **32** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichoja uvumba; **33** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^e **34** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^f **35** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^g alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Elisuri^h mwana wa Shedeuri.

36 Siku ya tano, mkuu wa wana wa Simeoni, Shelumeliⁱ mwana wa Zurishadai, **37** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^j vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^k **38** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichoja

uvumba; **39** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^a **40** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^b **41** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^c alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Shelumieli^d mwana wa Zurishadai.

42 Siku ya sita, mkuu wa wana wa Gadi, Eliasafu^e mwana wa Deueli, **43** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^f vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^g **44** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **45** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^h **46** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;ⁱ **47** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^j alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Eliasafu^k mwana wa Deueli.

SURA YA 7

a Law 1:3

b Law 4:22, 23

c Law 3:1

d Hes 1:4, 6

e Hes 2:14
Hes 10:20

f Law 27:25

g Law 2:1

h Law 1:3

i Law 4:22, 23

j Law 3:1

k Hes 1:4, 14

Safu ya 2

a Hes 2:18
Hes 10:22

b Law 27:25

c Law 2:1

d Law 1:3

e Law 4:22, 23

f Law 3:1

g Hes 1:4, 10

h Hes 2:20
Hes 10:23

i Law 27:25

j Law 2:1

48 Siku ya saba, mkuu wa wana wa Efraimu, Elishama^a mwana wa Amihudi, **49** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^b vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^c **50** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **51** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^d **52** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^e **53** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^f alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Elishama^g mwana wa Amihudi.

54 Siku ya nane, mkuu wa wana wa Manase, Gamalieli^h mwana wa Pedazuri, **55** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,ⁱ vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^j **56** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **57** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanako-

ndoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^a **58** mwambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^b **59** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^c alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Gamalieli^d mwana wa Pedazuri.

60 Siku ya tisa, mkuu^e wa wana wa Benjamini, Abidani^f mwana wa Gidioni, **61** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^g vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^h **62** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **63** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;ⁱ **64** mwambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^j **65** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^k alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Abidani^f mwana wa Gidioni.

66 Siku ya kumi, mkuu wa wana wa Dani, Ahiezeri^m mwana wa Amishadai, **67** alileta sahani moja ya fedha ye-

SURA YA 7

a Law 1:3

b Law 4:22, 23

c Law 3:1

d Hes 1:4, 10

e Hes 1:16

f Hes 2:22
Hes 10:24

g Law 27:25

h Law 2:1

i Law 1:3

j Law 4:22, 23

k Law 3:1

l Hes 1:4, 11

m Hes 2:25
Hes 10:25

Safu ya 2

a Law 27:25

b Law 2:1

c Law 1:3

d Law 4:22, 23

e Law 3:1

f Hes 1:4, 12

g Hes 2:27
Hes 10:26

h Law 27:25

i Law 2:1

j Law 1:3

nye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^a vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^b **68** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **69** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^c **70** mwambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^d **71** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^e alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Ahiezeri^f mwana wa Amishadai.

72 Siku ya 11, mkuu wa wana wa Asheri, Pagieli^g mwana wa Okrani, **73** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu,^h vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;ⁱ **74** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **75** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^j **76** mwambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya

dhambi;^a **77** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirika^b alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Pagielic mwana wa Okrani.

78 Siku ya 12, mkuu wa wana wa Naftali, Ahira^d mwana wa Enani, **79** alileta sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli 70 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatiifu,^e vyombo vyote viwili vilikuwa vimejaa unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka;^f **80** kikombe kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 10, kilichojaa uvumba; **81** ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa;^g **82** mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi;^h **83** na kwa ajili ya dhabihu ya ushirikaⁱ alileta ng'ombe wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano, na wanakondoo dume watano kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo yaliyokuwa matoleo ya Ahira^d mwana wa Enani.

84 Haya ndiyo matoleo ya kuzindua^k madhabahu yaliyolewa na wakuu wa Israeli siku ilipotiwa mafuta: sahani 12 za fedha, mabakuli 12 ya fedha, vikombe 12 vya dhahabu;^l **85** kila sahani ya fedha ilikuwa na uzito wa shekeli 130, na kila bakuli lilikuwa

SURA YA 7

a Law 4:22, 23

b Law 3:1

c Hes 1:4, 13

d Hes 2:29
Hes 10:27

e Law 27:25

f Law 2:1

g Law 1:3

h Law 4:22, 23

i Law 3:1

j Hes 1:4, 15

k Hes 7:10
Ezr 2:68

l Hes 7:13-17

Safu ya 2

a Law 27:25

b Hes 7:10

c Hes 7:1

d Kut 33:9
Hes 11:17
Hes 12:8e Kut 25:22
Kut 37:6f Kut 25:18
1Sa 4:4
Zb 80:1

SURA YA 8

g Kut 25:37
Kut 40:24, 25
Law 24:2

h Ebr 9:2

na uzito wa shekeli 70, fedha yote iliyotengeneza vyombo hivyo ilikuwa na uzito wa shekeli 2,400 kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatiifu;^a **86** vile vikombe 12 vya dhahabu vilivyojaa uvumba vilikuwa na uzito wa shekeli 10 kila kikombe kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatiifu, dhahabu yote iliyotengeneza vikombe hivyo ilikuwa na uzito wa shekeli 120. **87** Ng'ombe dume wote walioletwa kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa walikuwa 12, pia kondoo dume 12, wanakondoo dume 12 kila mmoja akiwa na umri wa mwaka mmoja na matoleo yao ya nafaka, na wanambuzi 12 kwa ajili ya dhabihu ya dhambi; **88** na ng'ombe dume wote walioletwa kwa ajili ya dhabihu ya ushirika walikuwa 24, pia kondoo dume 60, mbuzi dume 60, na wanakondoo dume 60 kila mmoja akiwa na umri wa mwaka mmoja. Hayo ndiyo matoleo yaliyotolewa kwa ajili ya kuizindua^b madhabahu baada ya kuitia mafuta.^c

89 Kila mara Musa alipoingia katika hema la mkutano kungea na Mungu,^d alisikia sauti ikizungumza naye kutoka juu ya kifuniko^e cha sanduku la Ushahidi, kutoka kati kati ya wale makerubi wawili;^f Mungu aliongea naye.

8 Yehova akamwambia Musa: **2** "Mwambie hivi Haruni: 'Unapowasha taa, taa hizo saba zinapaswa kuangaza upande wa mbele wa kinara cha taa.'"^g **3** Basi Haruni akafanya hivi: Akawasha taa hizo ili ziangaze upande wa mbele wa kinara cha taa,^h kama Yehova alivyomwamu-

ru Musa. **4** Hivi ndivyo kinara cha taa kilivyotengenezwa: Kilitengenezwa kwa nyundo^a kwa kutumia dhahabu; kuanzia shina lake mpaka maua yake, kilitengenezwa kwa nyundo. Kinara hicho cha taa kilitengenezwa kulingana na maono^b ambayo Yehova alikuwa amemwonyesha Musa.

5 Yehova akazungumza tena na Musa, akamwambia: **6** "Wachukue Walawi kutoka miongoni mwa Waisraeli, uwatakase.^c **7** Hivi ndivyo unavyopaswa kuwatakasa: Wanyunyizie maji ya kutakasa dhambi, na ni lazima wajiinyoe mwili mzima kwa we-mbe, wafue mavazi yao, na kujitakasa.^d **8** Kisha watachukua ng'ombe dume mchanga^e na toleo lake la nafaka^f la unga laini uliochanganywa na mafuta, nawe utachukua ng'ombe dume mwingine mchanga kwa ajili ya dhabihu ya dhambi.^g **9** Utawapeleka Walawi mbele ya hema la mkutano na kuwakusanya Waisraeli wote.^h **10** Utakapowapeleka Walawi mbele za Yehova, Waisraeli wataweka mikono yao juu ya Walawi.ⁱ **11** Ni lazima Haruni awatoe* Walawi mbele za Yehova kama toleo la kutikiswa/ kutoka kwa Waisraeli, nao watatekeleza utumishi wa Yehova.^k

12 "Kisha Walawi wataweka mikono yao juu ya vichwa vya wale ng'ombe dume.^l Kisha watamtotea Yehova ng'ombe dume mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi na mwingine kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa ili kufunika dhambi^m

8:11 *Tnn., "awatikise," yaani, awafanye waende mbele na nyuma.

SURA YA 8

a Kut 37:17

b Kut 25:9,40
1Nya 28:12,19c Kut 29:4
Isa 52:11d Kut 30:18,19
Law 16:28
Hes 19:7

e Law 1:3

f Law 2:1

g Law 4:3

h Law 8:2,3

i Hes 3:9,41

j Law 7:30
Hes 8:21k Hes 1:50
Hes 3:6
2Nya 31:2

l Kut 29:10

m Law 1:4

Safu ya 2

a Hes 3:45
Hes 16:9

b Hes 3:12

c Kut 13:2,12
Law 27:26d Kut 12:29
Kut 13:15e Hes 3:9
Hes 18:6
1Nya 23:32
Eze 44:11f Hes 1:53
Hes 18:5
1Sa 6:19

zao. **13** Nawe utawasimamisha Walawi mbele ya Haruni na wanawe na kuwatoa* kwa Yehova kama toleo la kutikiswa. **14** Ni lazima uwatenge Walawi kutoka miongoni mwa Waisraeli, nao Walawi watakuwa wangu.^a **15** Kisha Walawi wataingia ndani ya hema la mkutano ili kutumikia. Hivyo ndivyo unavyopaswa kuwatakasa na kuwatoa* kama toleo la kutikiswa. **16** Kwa maana wao ni watu waliokabidhiwa, niliokabidhiwa kutoka miongoni mwa Waisraeli. Nitawachukua hao kwa ajili yangu badala ya wazaliwa wote wa kwanza* wa Waisraeli.^b **17** Kwa maana kila mzaliwa wa kwanza miongoni mwa Waisraeli ni wangu, awe mwanaadamu au mnyama.^c Niliwatakasili ili wawe wangu siku niliyomuua kila mzaliwa wa kwanza nchini Misri.^d **18** Nitawachukua Walawi badala ya wazaliwa wote wa kwanza wa Waisraeli. **19** Nitampa Haruni na wanawe Walawi hao wakiwa watu waliokabidhiwa kutoka miongoni mwa Waisraeli, ili watumikie katika hema la mkutano^e kwa niaba ya Waisraeli na kutoa dhabihu ya kufunika dhambi za Waisraeli, na ili Waisraeli wasipatwe na pigo lolote^f kwa sababu wao hukaribia mahali patakatifu."

20 Musa na Haruni na Waisraeli wote wakawatendea Walawi mambo hayo. Waisraeli waliwatendea Walawi kulingana na mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Musa awatendee. **21** Basi Walawi

8:13, 15 *Tnn., "kuwatikisa," yaani, kuwafanya waende mbele na nyuma.
8:16 *Au "kila kifungua mimba."

wakajitakasa na kufua mavazi yao,^a kisha Haruni akawatoa* kama toleo la kutikiswa mbele za Yehova.^b Halafu Haruni akatoa dhabihu ya kufunika dhambi zao ili kuwatakasaa.^c **22** Baada ya hayo, Walawi waliingia ili kutumikia katika hema la mkutano chini ya usimamizi wa Haruni na wanaawe. Waliwatendea kama Yehova alivyomwamuru Musa kuhusu Walawi.

23 Sasa Yehova akamwambia Musa: **24** “Jambo hili linawahusu Walawi: Mwanamume mwenye umri wa miaka 25 na zaidi atajiunga na wale wanaotumikia katika hema la mkutano. **25** Lakini baada ya umri wa miaka 50 atastaafu, hataendelea na utumishi huo. **26** Anaweza kuwasaidia ndugu zake wanaotumikia katika hema la mkutano, lakini hapaswi kupewa kazi humo. Hivyo ndivyo utakavyofanya kuhusu Walawi na majukumu yao.”^d

9 Yehova akazungumza na Musa katika nyika ya Sinai katika mwezi wa kwanza^e wa mwaka wa pili baada ya wao kutoka nchini Misri, akamwambia: **2** “Waisraeli wanapaswa kutayarisha dhabihu ya Pasaka^f wakati wake uliopangwa.^g **3** Siku ya 14 ya mwezi huo kabla ya giza kuingia,* mnapaswa kuitayarisha wakati wake uliopangwa. Mnapaswa kuitayarisha kulingana na sheria zake zote na utaratibu wake wote uliowekwa.”^h

4 Basi Musa akawaambia Waisraeli waitayarisha dha-

SURA YA 8

a Hes 8:7

b Hes 8:11

c Hes 8:12

d Hes 1:53
Hes 3:32
Hes 18:4

SURA YA 9

e Kut 40:2
Hes 1:1

f Kut 12:27

g Kut 12:3, 6
Law 23:5
Kum 16:1
1Ko 5:7

h Kut 12:8

Safu ya 2

a Hes 5:2
Hes 19:14, 16b Kut 18:15
Hes 15:33
Hes 27:1, 2c Law 7:21
Kum 16:2d Kut 25:22
Law 16:2
Zb 99:6

e Hes 5:2

f 2Nya 30:2, 15

g Kut 12:8

h Kut 12:10

i Kut 12:46
Zb 34:20
Yoh 19:36

bihi ya Pasaka. **5** Kwa hiyo wakaitayarisha dhabihu ya Pasaka katika nyika ya Sinai katika mwezi wa kwanza, siku ya 14 ya mwezi huo kabla ya giza kuingia.* Waisraeli walifanya mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Musa.

6 Sasa watu fulani hawakuwa safi kwa sababu waligusa mtu aliyekufa,^a hivyo hawangeweza kuitayarisha dhabihu ya Pasaka siku hiyo. Kwa hiyo wakaenda kumwona Musa na Haruni siku hiyo,^b **7** wakamwambia Musa: “Sisi si safi kwa sababu tumemgusa mtu aliyekufa. Kwa nini tukatazwe kumtolea Yehova dhabihu kwa wakati uliopangwa pamoja na Waisraeli wengine?”^c **8** Ndiipo Musa akawaambia: “Ngojehi hapo, acheni nione Yehova ataamuru nini kuwahusu.”^d

9 Yehova akamwambia Musa: **10** “Waambie hivi Waisraeli: ‘Mtu yeyote miongoni mwenu au miongoni mwa vizazi vye-nu vijavyo akijichafua kwa kumgusa mtu aliyekufa^e au akisafiri mbali, bado anapaswa kumtayarishia Yehova dhabihu ya Pasaka. **11** Watu hao wanapaswa kuitayarisha katika mwezi wa pili,^f siku ya 14 kabla ya giza kuingia.* Wanapaswa kuila pamoja na mikate isiyo na chachu na mbo-ga chungu.^g **12** Hawapaswi kuacha chochote mpaka asubuhi,^h wala hawapaswi kuvunja mfupa wowote wa dhabihu hiyo.ⁱ Wanapaswa kuitayarisha kulingana na sheria zote za Pasaka. **13** Lakini ikiwa mtu alikuwa safi au hakuwa amesafiri naye amepuza kuitayarisha dhabihu ya Pasaka, ni lazima mtu huyo aua-

8:21 *Tnn., “akawatikisa,” yaani, akawafanya waende mbele na nyuma. **9:3, 5, 11** *Tnn., “katikati ya zile jioni mbili.”

we kutoka kati ya watu wake^a kwa sababu hakumtolea Yehova dhabihu hiyo kwa wakati wake uliopangwa. Mtu huyo ataadhibiwa kwa sababu ya dhambi yake.

14 “Ikiwa unaishi na mgeni, anapaswa pia kumtayarisha Yehova dhabihu ya Pasaka.^b Anapaswa kuitayarisha kulingana na sheria na utaratibu uliowekwa wa Pasaka.^c Ninyi nyote mtafuata sheria moja, mkaaji mgeni pamoja na mwenyeji wa nchi.”^d

15 Siku ambayo hema la ibada lilijengwa,^e wingu lilifunika hema la ibada, yaani, hema la Ushahidi, lakini wakati wa jioni kitu kilichoonekana kama moto kilikaa juu ya hema hilo mpaka asubuhi.^f **16** Hivi ndivyo ilivyokuwa kila siku: Wingu hilo lilifunika hema wakati wa mchana, na kitu kilichoonekana kama moto kilikaa juu ya hema wakati wa usiku.^g **17** Kila mara wingu hilo lilipoinuka kutoka juu ya hema, Waisraeli waliondoka bila kukawia,^h na mahali ambapo wingu hilo lilisimama, hapo ndipo Waisraeli walipopiga kambi.ⁱ **18** Waisraeli waliondoka kwa agizo la Yehova, na kwa agizo la Yehova walipiga kambi.^j Waliendelea kupiga kambi muda wote ambao wingu hilo lilikaa juu ya hema la ibada. **19** Wingu hilo lilipokaa juu ya hema la ibada kwa siku nyingi, Waisraeli walimtii Yehova nao hawakuondoka.^k **20** Nyakati nyingine wingu hilo lilikaa juu ya hema la ibada kwa siku chache. Waliendelea kupiga kambi kwa agizo la Yehova, na kwa agizo la Yehova walio-

SURA YA 9

a Kut 12:15

b Kut 12:19, 48

c Kut 12:8

d Law 24:22
Kum 31:12

e Kut 40:2, 17

f Kut 40:34, 38

g Kut 13:22
Ne 9:19

h Hes 10:11, 34

i Kut 40:36, 37

j Kut 17:1
Hes 10:11-13

k Kut 40:37

Safu ya 2

a Kut 40:36
Zb 78:14

SURA YA 10

b Law 23:24

c Hes 1:18
Kum 29:10, 11d Kut 18:21
Hes 1:16
Hes 7:2
Kum 1:15
Kum 5:23

e Hes 2:3

f Hes 2:10

ndoka. **21** Nyakati fulani wingu hilo lilikaa juu ya hema la ibada kuanzia jioni mpaka asubuhi tu, na wingu hilo lilipoinuka asubuhi, waliondoka. Iwe liliinuka mchana au usiku, waliondoka.^a **22** Iwe ni kwa siku mbili, mwezi mmoja, au muda mrefu zaidi, muda wote ambao wingu hilo lilikaa juu ya hema la ibada, Waisraeli waliendelea kupiga kambi nao hawakuondoka. Lakini lilipoinuka waliondoka. **23** Walipiga kambi kwa agizo la Yehova, na kwa agizo la Yehova waliondoka. Walitimiza wajibu wao kwa Yehova kama Yehova alivyowaagiza kupitia Musa.

10 Kisha Yehova akamwambia Musa: **2** “Jitegenezee tarumbeta mbili^b za fedha; zitengeneze kwa kutumia nyundo, nawe uzitumie kuwakusanya watu na kuvunja kambi. **3** Tarumbeta zote mbili zikipigwa, ni lazima Waisraeli wote wakusanyike mbele yako kwenye mlango wa hema la mkutano.^c **4** Tarumbeta moja tu ikipigwa, ni wakuu peke yao watakaokusanyika mbele yako, yaani, viongozi wa maelfu katika Israeli.^d

5 “Mkipiga tarumbeta kwa mlio unaobadilika-badilika, wale wanaopiga kambi upande wa mashariki^e wanapaswa kuanza safari. **6** Mkipiga tarumbeta mara ya pili kwa mlio unaobadilika-badilika, wale wanaopiga kambi upande wa kusini^f wanapaswa kuanza safari. Tarumbeta inapaswa kupigwa kwa njia hiyo kila mara kambi moja inapoanza safari.

7 “Mnapowakusanya watu wote, mnapaswa kuzipiga

tarumbeta^a kwa mlio usio-badilika-badilika. **8** Wana wa Haruni, makuhani, wanaswa kuzipiga tarumbeta;^b na hiyo itakuwa sheria ya kudumu katika vizazi vyenu vyote.

9 “Ikiwa maadui wanaowa-kandamiza watawashambulia katika nchi yenu, mnapaswa kupiga mwito wa vita kwa tarumbeta hizo,^c na Yehova Mungu wenu atawakumbuka na kuwaokoa kutoka kwa maadui wenu.

10 “Pia, katika siku zenu za kushangilia^d—wakati wa she-rehe zenu^e na mwanzoni mwa miezi yenu—mtazipiga tarumbeta hizo mnapotoa* dhahihu zenu za kuteketezwa^f na dhahihu zenu za ushirika;^g zitaniyana mimi Mungu wenu niwakumbuke. Mimi ni Yehova Mungu wenu.”^h

11 Basi katika mwaka wa pili, mwezi wa pili, siku ya 20 ya mwezi huo,ⁱ lile wingu lilinuka kutoka juu ya hema/ la Ushahidi. **12** Kwa hiyo Waisraeli wakaanza kuondoka katika nyika ya Sinai kulingana na utaratibu uliowekwa wa kuondoka,^k na wingu hilo likasimama katika nyika ya Parani.^l **13** Hiyo ilikuwa mara ya kwanza kwao kuondoka kama Yehova alivyokuwa amewaagiza kupitia Musa.^m

14 Kwa hiyo kundi la makabila matatu katika kambi ya wana wa Yuda liliondoka kwanza kulingana na vikosi vyake,^{*} na kiongozi wa kundi hilo alikuwa Nashoniⁿ mwana wa Aminadabu. **15** Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Isakari alikuwa Nethaneli^o

10:10 *Tnn., “juu ya.” 10:14, 18, 22, 25 *Tnn., “majeshi yake.”

SURA YA 10

a Hes 10:3

b Hes 31:6
1Nya 15:24
1Nya 16:6
2Nya 29:26
Ne 12:35, 41

c 2Nya 13:12

d 1Nya 15:28
2Nya 5:12
2Nya 7:6
Ezr 3:10

e Law 23:24
Hes 29:1

f Hes 28:11

g Law 3:1

h Kut 6:7
Law 11:45

i Hes 1:1

j Hes 9:17
Zb 78:14

k Kut 40:36
Hes 2:9, 16, 17,
24, 31

l Hes 12:16
Hes 13:26
Kum 1:1, 2

m Hes 2:34
Hes 9:23

n Hes 1:4, 7
Hes 2:3

o Hes 1:4, 8
Hes 2:5

Safu ya 2

a Hes 2:7

b Hes 1:51

c Hes 3:25, 26

d Hes 3:36, 37

e Hes 1:4, 5
Hes 2:10

f Hes 1:5, 6
Hes 2:12

g Hes 1:4, 14
Hes 2:14

h Hes 3:30, 31
Hes 4:15
Hes 7:9

i Hes 1:4, 10
Hes 2:18, 24

j Hes 1:4, 10
Hes 2:20

k Hes 1:4, 11
Hes 2:22

l Hes 1:4, 12
Hes 2:25, 31

m Hes 1:4, 13
Hes 2:27

mwana wa Zuari. **16** Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Zabuloni alikuwa Eliabu^a mwana wa Heloni.

17 Hema la ibada lilipofunguliwa,^b wana wa Gershoni^c na wana wa Merari,^d waliobeba hema hilo, walianza safari.

18 Kisha kundi la makabila matatu katika kambi ya Rubeni liliondoka kulingana na vikosi vyake,^{*} na kiongozi wa kundi hilo alikuwa Elisuri^e mwana wa Shedeuri. **19** Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Simeoni alikuwa Shelumieli^f mwana wa Zuri-shadai. **20** Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Gadi alikuwa Eliasafu^g mwana wa Deueli.

21 Kisha Wakohathi, walio-beba vyombo vya mahali patakatiifu,^h wakaondoka. Hema la ibada lilipaswa kusimami-shwa kabla hawajafika.

22 Kisha kundi la makabila matatu katika kambi ya wana wa Efraimu liliondoka kulingana na vikosi vyake,^{*} na kiongozi wa kundi hilo alikuwa Elishamaⁱ mwana wa Amihudi. **23** Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Manase alikuwa Gamalieli^j mwana wa Pedazuri. **24** Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Benjamini alikuwa Abidani^k mwana wa Gidioni.

25 Kisha kundi la makabila matatu katika kambi ya wana wa Dani liliondoka kulingana na vikosi vyake,^{*} nao walikuwa kikosi cha nyuma cha kulingana na kiongozi wa kundi hilo alikuwa Ahiezeri^l mwana wa Amishadai.

26 Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Asheri alikuwa Pagieli^m mwana wa Okrani.

27 Kiongozi wa kikosi cha kabila la wana wa Naftali alikuwa Ahira^a mwana wa Enani.

28 Huo ndio utaratibu ambao Waisraeli na vikosi vyao walifuata* kila mara walipoanza safari.^b

29 Kisha Musa akamwambia Hobabu mwana wa Reueli,^{*c} Mmidiani, baba mkwe wake: “Tunaenda mahali ambapo Yehova alisema, ‘Nitawapa ninyi mahali hapo.’^d Basi twende pamoja,^e nasi tutakutendea mema, kwa sababu Yehova ameahidi kuwapa Waisraeli mambo mema.”^f

30 Lakini akamwambia: “Sitaenda. Nitarudi katika nchi yangu na kwa watu wangu wa ukoo.” **31** Musa akamwambia: “Tafadhali usituache, kwa maana unajua mahali tunapopaswa kupiga kambi nyikani, nawe unaweza kutuonyesha njia.* **32** Ukienda pamoja nasi,^g jambo lolote jema ambalo Yehova atatutendea, bila shaka tutakutendea wewe pia.”

33 Basi wakasafiri kwa siku tatu kutoka kwenye mlima wa Yehova,^h na sandukuⁱ la agano la Yehova lilisafirishwa mbele yao kwa siku hizo tatu ili kuwatafutia mahali pa kupumzika.^j **34** Nalo wingu la Yehova^k lilikuwa juu wakiwa wa mchana walipoondoka mahali walipokuwa wamepiga kambi.

35 Kila mara Sanduku hilo lilipoanza kusafirishwa, Musa alisema: “Inuka, Ee Yehova,^l acha maadui wako watawanyike, na wale wanaokuchukia wakimbie kutoka mbele zako.”

10:28 *Tnn., “majeshi yao yalifuata.”

10:29 *Yaani, Yethro. 10:31 *Tnn., “kuwa macho yetu.”

SURA YA 10

a Hes 1:4, 15
Hes 2:29

b Hes 2:34

c Kut 2:16, 18
Kut 3:1
Kut 18:1, 5

d Mwa 12:7
Mwa 13:14, 15
Mwa 15:18

e Amu 1:16
Amu 4:11
1Sa 15:6

f Kut 3:8
Kut 6:7

g Amu 1:16
Amu 4:11

h Kut 3:1
Kut 19:3
Kut 24:16
Kum 5:2

i Kut 25:10, 17

j Kum 1:32, 33
Yos 3:3, 4

k Kut 13:21
Ne 9:12
Zb 78:14

l Zb 132:8

Safu ya 2

a Kum 1:10

SURA YA 11

b Kut 32:11
Kum 9:19
Zb 106:23
Yak 5:16

c Kum 9:22

d Kut 12:37, 38
Law 24:10

e 1Ko 10:6, 10

f Zb 78:18, 22
Zb 106:14

g Kut 16:3

h Kut 16:35
Hes 21:5

i Kut 16:14
Ne 9:20
Yoh 6:31

j Kut 16:31

36 Na lilipowekwa chini, alisema: “Rudi, Ee Yehova, kwa maelfu yasiyohesabika* ya Waisraeli.”^a

11 Sasa watu wakaanza kulalamika kwa uchungu mbele za Yehova. Yehova aliposikia malalamiko yao, alikasirika sana, na moto kutoka kwa Yehova ukaanza kuwateketeza na kuwaangamiza baadhi ya watu waliokuwa kandokando ya kambi. **2** Watu walipoanza kumlilia Musa, alimwomba Yehova dua,^b nao moto ukazimika. **3** Kwa hiyo mahali hapo pakaitwa Tabera,^{*c} kwa sababu moto kutoka kwa Yehova uliwateketeza watu.^c

4 Kisha umati wa watu waliochangamana nao^{*d} ukaanza kutamani chakula kwa pupa,^e basi Waisraeli wakaaanza kulia tena na kusema: “Ni nani atakayetupatia nyama tule?^f **5** Tunakumbuka sana samaki wa bure tuliokuwa tukila nchini Misri, pamoja na matango, matikiti, vitunguu vya majani, vitunguu maji, na vitunguu saumu!^g **6** Lakini sasa tunadhoofika. Hatuoni kitu kingine chochote isipo-kuwa hii mana.”^h

7 Kwa kweli, manaⁱ ilikuwa kama mbegu za giligilani,^j na ilionekana kama utomvu wa mbedola. **8** Watu walikuwa wakienda kila mahali kuiokota, kisha waliisaga kwa mawe ya kusagia au waliitwanga kwenye kinu. Hala- fu waliichemsha katika vyyungu vya kupikia au waliitumia

10:36 *Au “makumi ya maelfu kwa maelfu.” 11:3 *Maana yake “Kuteketea,” yaani, moto mkali. 11:4 *Inaonekana ni watu ambao hawakuwa Waisraeli.

kuoka mikate ya mviringo,^a na ladha yake ilikuwa kama ladha ya keki tamu iliyoookwa kwa mafuta. **9** Umande ulipoanguka kambini usiku, mana pia ilianguka pamoja na umande huo.^b

10 Musa akawasikia watu wakilia katika kila familia, kila mtu kwenye mlango wa hema lake. Basi Yehova akakasirika sana,^c na Musa pia akachukizwa sana na jambo hilo. **11** Kisha Musa akawambia Yehova: "Kwa nini unanitesa mimi mtumishi wako? Kwa nini hupendezwi nami, hivi kwamba umenitwika mzigo wa watu wote hawa?^d

12 Je, ni mimi niliyebeba mimba ya watu hawa wote? Je, ni mimi niliyewazaa ndiyo sababu unaniambia, 'Wabebe kifuani pako, kama mlezi*' anavyombeba mtoto mchanga,' na kuwapeleka katika nchi uliyoapa kwamba utawapa mababu zao?^e **13** Nitapata wapi nyama ya kuwapa watu hawa wote? Kwa sababu wanaendelea kunililia wakisema, 'Tupe nyama tule!' **14** Siwezi kuwabeba watu hawa wote peke yangu; ni mzigo mzito sana kwangu.^f **15** Ikiwa utaendelea kunitendea hivi, tafadhali niue sasa hivi.^g Ikiwa nimepata kibali machoni pako, usiache niendeleo kutaabika."

16 Yehova akamjibu Musa: "Nikusanyie wanaume 70 miongoni mwa wazee wa Israeli, wanaume ambao unajua kwamba ni wazee na maofisa wa watu,^h nawe uwapeleke kwenye hema la mkutano, na kuwaagiza wasimame hapo pa-

SURA YA 11

a Kut 16:16, 23

b Zb 78:24

c Hes 11:1

d Kut 17:4
Kum 1:12e Mwa 13:14, 15
Mwa 26:3f Kut 18:17, 18
Kum 1:9g 1Fa 19:2, 4
Ayu 6:8, 9

h Kum 16:18

Safu ya 2

a Kut 19:11
Kut 25:22
Kut 34:5
Hes 12:5b Hes 11:25
Hes 12:8c 1Sa 10:6
2Fa 2:15
Ne 9:20
Mdo 2:17

d Kut 18:21, 22

e Kut 19:10

f Kut 16:7

g Hes 11:4, 5

h Kut 16:8

i Zb 78:29

j Hes 11:5

k Kut 12:37
Kut 38:26
Hes 1:45, 46l Mwa 18:14
Isa 59:1
Mk 10:27
Lu 1:37

moja nawe. **17** Nitashuka^a na kuzungumza nawe hapo,^b nami nitachukua kiasi fulani cha roho^c iliyo juu yako na kuiweka juu yao, nao watakusaidia kubeba mzigo wa watu hawa ili usiubebe peke yako.^d **18** Unapaswa kuwaambia watu, 'Jitakaseni kwa ajili ya kesho,^e kwa maana hakika mtakula nyama, kwa sababu Yehova amewasikia mkilia^f na kusema: "Ni nani atakayetupatia nyama tule? Hali yetu ilikuwa nzuri zaidi nchini Misri."^g Hakika Yehova atawapa nyama, nanyi mtaila.^h **19** Hamtaila kwa siku moja tu, au siku 2, au siku 5, au siku 10, au hata siku 20, **20** bali kwa mwezi mzima, mpaka itakapotokea kwenye mianzi ya pua zenu na kuwachukiza,ⁱ kwa sababu mlimekataa Yehova aliye kati yenu, nanyi mlilia mbele zake mkisema: "Kwa nini tumetoka Misri?"^j

21 Kisha Musa akasema: "Niko miongoni mwa wanaume 600,000^k wanaotembea kwa miguu, nawe unasema, 'Nitawapa nyama, nao watakula nyama ya kutosha kwa mwezi mzima!' **22** Je, maku-ndi mazima ya kondoo na ng'ombe yakichinjwa, yatawatosha? Au samaki wote wa baharini wakivuliwa, je, watawatosha?"

23 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Je, mkono wa Yehova ni mfupi?^l Sasa utaona ikiwa jambo ninalosema litati-mia kwako au la."

24 Basi Musa akatoka na kuwaambia watu maneno ya Yehova. Akawakusanya wanaume 70 miongoni mwa wazee wa watu na kuwaagiza wa-

simame kuzunguka hema la mkutano.^a **25** Kisha Yehova akashuka katika wingu^b na kuzungumza naye,^c akachukua kiasi fulani cha roho^d iliyokuwa juu yake na kuiweka juu ya kila mmoja wa wale wazee 70. Na mara tu roho hiyo iliposhuka juu yao, wakaanza kutenda kama manabii,^{*e} lakini hawakufanya hivyo tena.

26 Wawili kati ya wanaume hao walibaki kambini. Mmoja aliitwa Eldadi na mwingine Medadi. Na roho ikaanza kushuka juu yao, kwa maana walikuwa kati ya wale ambao majina yao yalikuwa yameandikwa lakini hawakwenda kwenye hema la mkutano. Basi wakaanza kutenda kama manabii kambini. **27** Mwanamume mmoja kijana akakimbia na kumwambia Musa: "Eldadi na Medadi wanatenda kama manabii kambini!" **28** Ndipo Yoshua^f mwana wa Nuni, aliyekuwa mtumishi wa Musa tangu ujanani, akasema: "Bwana wangu Musa, wakataze!"^g **29** Lakini Musa akamwambia: "Je, unaona wivu kwa ajili yangu? Usifanye hivyo, laiti watu wote wa Yehova wangekuwa manabii na laiti Yehova angeweka roho yake juu yao!" **30** Baadaye Musa akarudi kambini pamoja na wazee wa Israeli.

31 Kisha upepo kutoka kwa Yehova ukavuma ghafla na kuanza kuleta kware kutoka baharini na kuwaangusha kote kote kambini,^h kwenye eno la umbali wa siku moja hivi kila upande kuzunguka kamibi, wakafikia kimo cha miko-

11:25 *Au "wakaanza kutabiri."

SURA YA 11

a Hes 11:16

b Kut 33:9
Hes 12:5
Kum 31:15

c Zb 99:7

d Hes 11:17
Zfa 2:9, 15

e 1Sa 10:6
1Sa 19:20

f Kut 17:9
Kut 24:13
Kut 33:11
Hes 27:18-20
Kum 31:3

g Mk 9:38

h Kut 16:13
Zb 78:26, 27

Safu ya 2

a Zb 78:30, 31
1Ko 10:10

b Hes 33:16
Kum 9:22

c 1Ko 10:6

d Hes 33:17

SURA YA 12

e Kut 2:16, 21

f Kut 4:14-16
Kut 4:30
Kut 15:20
Kut 28:30
Mik 6:4

g Hes 11:1

h Mt 11:29

no miwili* hivi kutoka ardhi ni. **32** Basi siku hiyo yote, mchana na usiku wote, na siku nzima iliyofuata waliendelea kuokota kware. Hakuna aliyekota chini ya homeri kumi,* nao waliwaanika kila mahali kambini. **33** Lakini nyama ilipokuwa ingali kati kati ya meno yao, kabla hawajaitafuna, hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya watu, na Yehova akaanza kuwapiga watu kwa maangamizi makubwa sana.^a

34 Kwa hiyo wakapaita mahali hapo Kibroth-hataava,^{*b} kwa sababu hapo ndipo walipowazika watu waliokuwa na tamaa na pupa.^c **35** Kutoka Kibroth-hataava watu wakasafiri mpaka Haserothi^d na ku-kaa huko.

12 Miriamu na Haruni wakaanza kusema vibaya kumhusu Musa kwa sababu ya mwanamke Mkushi aliyekuwa amemwoa, kwa maana Musa alikuwa ameoa mwanamke Mkushi.^e **2** Walikuwa wakisema: "Je, Yehova amezungumza kupitia Musa peke yake? Je, hajazungumza kupitia sisi pia?"^f Na Yehova alikuwa akisikiliza.^g **3** Basi Musa alikuwa mtu mpole zaidi kuliko watu wote^{*h} duniani.

4 Kwa ghafla Yehova akamwambia Musa, Haruni, na Miriamu: "Ninyi watatu, nendeni kwenye hema la

11:31 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. **11:32** *Homeri ni kipimo sawa na lita 220. Angalia Nyongeza B14. **11:34** *Maana yake "Makaburi ya Watu Wenye Tamaa." **12:3** *Au "mnyenyekevu zaidi, kuliko mtu mwingine yeyote."

mkutano.” Basi wote wata-tu wakaenda. **5** Yehova aka-shuka katika nguzo ya wingu^a na kusimama kwenye mlango wa hema la mkutano, akamwita Haruni na Miriamu. Wote wawili wakaenda mbele. **6** Ndipo akawaambia: “Tafadhali, sikilizeni maneno yangu. Ikiwa nabii wangu, mimi Yehova, angekuwa miongoni mweni, ningejitambulisha kwake katika maono,^b nami ningengea naye katika ndoto.^c **7** Lakini sijafanya hivyo kuhusiana na mtumishi wangu Musa! Nimemkabidhi nyumba yangu yote.^{*d} **8** Mimi huongea naye uso kwa uso,^{*e} waziwazi, wala si kwa mafumbo; naye huona uwepo wangu, mimi Yehova. Kwa nini, basi, hamkuogopa kusema vibaya kumhusu Musa, mtumishi wangu?”

9 Kwa hiyo hasira ya Yehova ikawaka dhidi yao, naye akaenda zake. **10** Lile wingu likaondoka juu ya hema, na tazama! Miriamu alikuwa amepigwa kwa ukoma mweupe kama theluji.^f Kisha Haruni akaageuka na kumtazama Miriamu, akaona kwamba alikuwa amepigwa kwa ukoma.^g **11** Mara moja Haruni akamwambia Musa: “Nakusihi, bwana wangu! Tafadhali, usituadhibu kwa sababu ya dhambi hii! Tumetenda kwa upumbavu. **12** Tafadhali, usimwache aendelee kuwa kama mtu aliyezaliwa akiwa amekufa, ambaye nusu ya mwili wake imeozal!” **13** Basi Musa akaanza kumlilia Yehova, akisema: “Ee Mu-

12:7 *Tnn., “Anajithibitisha mwenyewe kuwa mwaminifu katika nyumba yangu yote.” 12:8 *Tnn., “kinywa kwa kinywa.”

SURA YA 12

a Kut 34:5
Hes 11:25

b Mwa 15:1
Mwa 46:2
Kut 24:9-11

c Mwa 31:10, 11

d Ebr 3:2, 5

e Kut 33:11
Kum 34:10

f Kum 24:9

g 2Nya 26:19

Safu ya 2

a Kut 32:11
Yak 5:16

b Law 13:45, 46
Hes 5:2

c Kum 24:9

d Hes 11:35
Hes 33:18

e Hes 10:12

SURA YA 13

f Kut 18:25
Kum 1:15

g Kum 1:22, 23

h Hes 12:16
Kum 1:19

i Hes 13:30
Hes 14:30, 38
Hes 34:18, 19
1Nya 4:15

j Hes 11:28
Hes 13:16
Hes 14:30
Hes 34:17

k Mwa 48:5

l Mwa 48:17, 19

ngu, tafadhali mponye! Tafadhali!”^a

14 Yehova akamjibu Musa: “Ikiwa baba yake angemtemea mate usoni moja kwa moja, je, hangeaibika kwa siku saba? Acha atengwe nje ya kambi kwa siku saba,^b kisha ana-weza kurudishwa kambini.” **15** Kwa hiyo Miriamu akatengwa nje ya kambi kwa siku saba,^c na watu hawakuendelea na safari hadi Miriamu aliporudishwa kambini. **16** Kisha watu wakaondoka Haserothi^d na kuanza kupiga kambi katika nyika ya Parani.^e

13 Yehova akamwambia Musa: **2** “Watume wanaume wakaipieleze nchi ya Kanaani ninayowapa Waisraeli. Mtume mwanamume mmoja kutoka katika kila kabila la baba yake, kila mmoja wao anapaswa kuwa mkuu^f katika kabila lake.”^g

3 Basi Musa akawatuma kutoka katika nyika ya Parani^h kama Yehova alivyomwagiza. Wanaume hao wote walikuwa viongozi wa Waisraeli. **4** Haya ndiyo majina yao: kutoka katika kabila la Rubeni, Shamua mwana wa Zakuri; **5** kutoka katika kabila la Simeoni, Shafati mwana wa Hori; **6** kutoka katika kabila la Yuda, Kalebⁱ mwana wa Yefune; **7** kutoka katika kabila la Isakari, Igali mwana wa Yosefu; **8** kutoka katika kabila la Efraimu, Hoshea^j mwana wa Nuni; **9** kutoka katika kabila la Benjamini, Palti mwana wa Rafu; **10** kutoka katika kabila la Zabuloni, Gadieli mwana wa Sodi; **11** kutoka katika kabila la Yosefu,^k kwa ajili ya kabila la Manase,^l Gadi mwana wa Susi;

12 kutoka katika kabila la Dani, Amieli mwana wa Gemali; 13 kutoka katika kabila la Asheri, Sethuri mwana wa Mikaeli; 14 kutoka katika kabila la Naftali, Nabi mwana wa Vofsi; 15 kutoka katika kabila la Gadi, Geuli mwana wa Maki. 16 Hayo ndiyo majina ya wanaume ambao Musa aliwatuma kuipeleleza nchi. Musa alimpa Hoshea mwana wa Nuni jina Yoshua.*^a

17 Musa alipokuwa akiwatumia kuipeleleza nchi ya Kanaani, aliwaambia: "Pandeni mwingie Negebu, na kwenda juu kwenye eneo lenye milima.^b 18 Chunguzeni mwone nchi hiyo ilivyo^c na kama watu wanaoishi humo ni wenyewe nguvu au dhaifu, wengi au wachache, 19 na kama nchi hiyo ni nzuri au ni mbaya na kama majiji wanamoishi ni kambi au ni ngome. 20 Chunguzeni ikiwa ni nchi tajiri au maskini,^d ina miti au haina. Ni lazima muwe jasiri^e na kuchukua baadhi ya matunda ya nchi hiyo." Ulikuwa wakati wa kuiva kwa zabibu za kwanza.^f

21 Basi wakaenda na kuipeleleza nchi kuanzia nyika ya Zini^g hadi Rehobu,^h karibu na Lebo-hamathi.*ⁱ 22 Walipopanda na kuingia Negebu, walifika Hebroni,^j ambako Ahimani, Sheshai, na Talmi,^k wazao wa Anaki^l waliishi. Sasa, Jiji la Hebroni lilijengwa miaka saba kabla ya jiji la Soani lililoko Misri. 23 Walipofika kwenye Bonde la Eshkoli,^m walikata tawi lenye kishada kimoja cha zabibu, na wanaume wa-

13:16 *Au "Yehoshua," linalomaanisha Yehova Ni Wokovu. 13:21 *Au "nija ya kuingia Hamathi."

SURA YA 13

a Kut 17:9

b Kum 1:7

c Kut 3:8
Kum 8:7d Ne 9:25
Eze 20:6e Kum 31:6
Yos 1:6, 9

f Hes 13:23

g Hes 34:2, 3
Yos 15:1

h 2Sa 10:6, 8

i Hes 34:8

j Mwa 13:18
Yos 15:13
Yos 21:11, 12

k Amu 1:10

l Kum 9:1, 2
Yos 11:21

m Hes 32:9

Safu ya 2

a Kum 1:25
Kum 8:7-9

b Kum 1:24

c Hes 14:33, 34

d Kum 1:19

e Kut 3:8
Law 20:24

f Kum 1:25

g Hes 13:22, 33
Kum 1:27, 28h Mwa 36:12
Kut 17:8
1Sa 15:3

i Hes 13:17

j Amu 1:21
2Sa 5:6, 7

k Mwa 10:15, 16

l Kut 23:23
Kum 7:1
Kum 20:17

m Mwa 10:19

n Yos 14:7, 8

o Hes 32:9

p Hes 14:36

wili wakalibeba kwa ufito pamoja na makomamanga kadhaa na tini.^a 24 Wakapaita mahali hapo Bonde la Eshkoli*^b kwa sababu ya kishada ambacho Waisraeli walikata kutoka huko.

25 Baada ya kuipeleleza nchi kwa siku 40,^c wanau-me hao walirudi. 26 Walirudi kwa Musa, Haruni, na Waisraeli wote katika nyika ya Parani, huko Kadeshi.^d Wakawaleta habari Waisraeli wote na kuwaonyesha matunda ya nchi hiyo. 27 Hivi ndivyo walivyomwambia Musa: "Tuliingia katika nchi uliyotutuma, na kwa kweli inatiririka maziwa na asali,^e na haya ndiyo matunda yake.^f 28 Lakini watu wanaoishi katika nchi hiyo wana nguvu, na majiji yao yenye ngome ni makubwa sana. Tuliona pia wazao wa Anaki huko.^g 29 Waamaleki^h wanaishi katika nchi ya Negebu,ⁱ nao Wahiti, Wayebusi,^j na Waamori^k wanaishi katika eneo lenye milima, na Wakanaani^l wanaishi karibu na bahari^m na kwenye kingo za Yordani."

30 Kisha Kalebu akajaribu kuwatuliza watu waliosimama mbele ya Musa kwa kuwaambia: "Twendeni mara moja, na bila shaka tutaimiliki, kwa maana kwa hakika tunaweza kuishinda."ⁿ 31 Lakini wanaume waliopanda huko pamoja naye wakasema: "Hatuwezi kwenda kupigana na watu hao, kwa sababu wana nguvu kuliko sisi."^o 32 Nao wakaendelea kuwapa Waisraeli habari mbaya^p kuhusu nchi waliyoipeleleza, wakisema:

13:24 *Maana yake "Kishada cha Zabibu."

“Nchi tuliyoenda kuipeleleza ni nchi inayowameza wakaaji wake, na watu wote tuliowao-na huko ni wakubwa isivyo kawaida.^a **33** Na huko tuliwao-na Wanefili, wana wa Anaki,^b wazao wa Wanefili, tulijiona kuwa kama panzi mbele yao, na ndivyo walivyotuona.”

14 Basi Waisraeli wote wakalia kwa sauti na kutokwa na machozi usiku kucha.^c **2** Waisraeli wote wakaanza kumnung'unikia Musa na Haruni,^d na wote wakawalalamikia wakisema: “Laiti tungalifia katika nchi ya Misri, au laiti tungalifia hapa nyikani! **3** Kwa nini Yehova anatuleta kwenye nchi hii ili tuawe kwa upanga?^e Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka.^f Je, si afadhali turudi Misri?”^g **4** Hata waliambia-na: “Na tuchague kiongozi, turudi Misri!”^h

5 Ndipo Musa na Haruni wakaanguka chini kifudufudi mbele ya Waisraeli wote waliokuwa wamekusanyika. **6** Yohshuaⁱ mwana wa Nuni na Kalebu^j mwana wa Yefune, waliokuwa miongoni mwa watu walioipeleleza nchi, wakayararua mavazi yao, **7** na kuwambia hivi Waisraeli wote: “Nchi tuliyoenda kuipeleleza ni nchi nzuri sana, nzuri kwelikweli.^k **8** Ikiwa Yehova amependezwa nasi, kwa hakika atatuungiza katika nchi hii na kutupatia iwe yetu, nchi inayotiririka maziwa na asali.^l **9** Lakini msimwasi Yehova, nanyi msiwaogope watu wa nchi hiyo,^m kwa maana tutawashinda kwa urahisi.* Ulinzi wao umeondo-

14:9 *Tnn., “wao ni mkate kwetu.”

SURA YA 13

a Amo 2:9

b Kum 1:28
Kum 9:1, 2

SURA YA 14

c Kum 1:32, 33

d Kum 1:27
Zb 106:25

e Zb 78:40

f Hes 14:31
Kum 1:39

g Hes 11:5

h Ne 9:17

i Hes 13:8, 16

j Hes 13:6, 16
Hes 14:30

k Hes 13:26, 27
Kum 1:25
Kum 6:7, 8

l Kut 3:8

m Kum 7:17, 18
Kum 20:3

Safu ya 2

a Kut 33:16
Kum 20:1

b Kut 17:4

c Kut 16:10

d Kut 16:28
Hes 14:22, 23

e Kum 9:23
Ebr 3:19

f Kut 32:10

g Kut 32:12
Eze 20:9

h Kut 15:13, 14
Yos 2:10
Yos 5:1

i Kum 4:12
Kum 5:4

j Kut 13:21
Zb 78:14

k Kum 9:28

lewa, na Yehova yuko pamoja nasi.^a Msiwaogope.”

10 Hata hivyo, Waisraeli wote wakasema wapigwe mawe.^b Lakini utukufu wa Yehova ukatokea juu ya hema la mkutano machoni pa Waisraeli wote.^c

11 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Watu hawa wataendelea kunidharau mpaka lini,^d watakataa kuniامي ni mpaka lini licha ya miujiza yote niliyofanya miongoni mwao?^e **12** Acha niwapige kwa ugonjwa hatari* na kuwafukuza, na acha nikufanye wewe kuwa taifa kubwa zaidi na lenye nguvu zaidi kuliko wao.”^f

13 Lakini Musa akamwambia Yehova: “Kisha Wamisri, ambao kati yao uliwa-toa watu hawa kwa nguvu zako, watasikia habari hizo,^g

14 nao watawambia wakaaji wa nchi hii. Wakaaji hao pia wamesikia kwamba wewe, Yehova, uko miongoni mwa watu hawa,^h nawe umewatokea uso kwa uso.ⁱ Wewe ni Yehova, na wingu lako limesimama juu yao, nawe unawatangulia katika nguzo ya wingu wakati wa mchana na katika nguzo ya moto wakati wa usiku.^j **15** Ukiwaua watu hawa wote mara moja, mataifa ambayo yamesikia sifa zako yatasema, **16** ‘Yehova alishindwa kuwapeleka watu hawa katika nchi ambayo alipa kuwa angewapa ndiyo sababu aliwachinja nyikani.’^k

17 Sasa, Ee Yehova, tafadhali, acha nguvu zako kuu zionekane, kama ulivyoahidi uliposema, **18** ‘Mimi Yehova,

14:12 *Au “tauni.”

si mwepesi wa hasira, nina upendo mwingi mshikamanifu,*^a ninasamehe makosa na uovu, lakini sikosi kamwe kuwaadhibu wenye hatia, nina-waadhibu wana na wajukuu kufikia kizazi cha tatu na channe kwa sababu ya makosa ya baba zao.^b **19** Tafadhali, wasamehe watu hawa dhambi zao kulingana na upendo wako mwingi mshikamanifu, kama ambavyo umekuwa ukivasamehe tangu walipotoka Misri mpaka sasa.”^c

20 Basi Yehova akasema: “Nimewasamehe kama ulivyoomba.^d **21** Lakini, kwa hakika kama niishivyo, dunia yote itajaa utukufu wa Yehova.^e **22** Hata hivyo, hakuna mtu hata mmoja aliyeona utukufu wangu na miujiza^f niliyofanya nchini Misri na nyikani ambaye bado ananijaribu^g mara hizi kumi na kukataa kusikiliza sauti yangu^h **23** ataiona nchi niliyoapa kwamba nitawapa baba zao. Hakuna mtu hata mmoja anayenidharau atakayeiona.ⁱ **24** Lakini kwa sababu mtumishi wangu Kalebu^j alikuwa na roho tofauti naye aliendelea kunifuata kwa moyo wote, kwa hakika nitamwingiza katika nchi aliyoenda kuipeleleza, na wazao wake wataimiliki.^k **25** Kwa kuwa Waamaleki na Wakanaani^l wanaishi bonde-ni, kesho geukeni mwelekee nyikani kupitia njia ya Bahari Nyekundu.”^m

26 Kisha Yehova akamwambia Musa na Haruni: **27** “Umati huu wa watu waovu utae-ndelea kuninung'unikia mpa-

14:18 *Au “fadhili nyingi zenye upendo.”

SURA YA 14

a Zb 103:8

Mik 7:18

b Kut 34:6,7

c Kut 34:9

Zb 78:38

d Yak 5:16

e Zb 72:19

Hab 2:14

f Ne 9:17

g Kut 17:2

Zb 95:9

Zb 106:14

Ebr 3:16

h Zb 81:11

i Hes 26:63, 64

Hes 32:11

Kum 1:35

Zb 95:11

Zb 106:26

Ebr 3:18

Ebr 4:3

j Hes 13:30

Hes 26:65

k Yos 14:9,14

l Hes 13:29

m Kum 1:40

Safu ya 2

a Kut 16:28

Hes 14:11

b 1Ko 10:6,10

c Hes 14:2

Hes 26:64

Hes 32:11

Kum 1:35

d Zb 106:26

1Ko 10:5

Ebr 3:17

e Hes 1:45, 46

Yud 5

f Kut 6:8

g Hes 26:65

Hes 32:11, 12

Kum 1:34-38

h Hes 14:3

Kum 1:39

i Zb 106:24

j Hes 32:13

Yos 14:10

k Kum 1:3

Kum 2:14

l Zb 95:10

Mdo 7:36

Mdo 13:18

m Hes 13:25

n Hes 14:29

Ebr 3:17

ka lini?^a Nimesikia manung'uniko ya Waisraeli juu yangu.^b

28 Waambie, “Kwa hakika kama ninavyoishi,” asema Yehova, “nitawatendea mambo yaleyale niliyosikia mkisema!^c

29 Maiti zenu zitaanguka katika nyika hii,^d naam, ninyi nyote mlioninung'unikia, kila mtu aliyeandikishwa mwenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi.^e

30 Hakuna hata mmoja wenu atakayeingia katika nchi niliyoapa kwamba mtaishi ndani yake,^f isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune na Yoshua mwana wa Nuni.^g

31 ““Na watoto wenu ambao mlisema kwamba watakuwa mateka,^h nitawaingiza katika nchi ambayo mmeikataa, nao wataijua.ⁱ **32** Lakini maiti zenu zitaanguka katika nyika hii. **33** Wana wenu watakuwa wachungaji nyikani kwa miaka 40,^j nao lazima wateseke kwa sababu ya mate-ndo yenu ya kukosa uaminifu* mpaka mtu wenu wa mwisho atakapofia nyikani.^k **34** Mta-teseka kwa sababu ya makosa yenu kwa miaka 40,^l sawa na siku 40^m ambazo mliipeleleza nchi, yaani, siku moja kwa mwaka mmoja, siku moja kwa mwaka mmoja, kwa maana mtajionea matokeo ya kunipinga mimi.*

35 ““Mimi, Yehova, nimesema. Hivi ndivyo nitakavyo-ndeenda umati huu wa watu waovu, ambao umekusanyika pamoja dhidi yangu: Wataishia humu nyikani, naam, watafia humu.ⁿ **36** Wanaume ambao Musa aliwatuma kuipeleleza nchi, wakaleta habari mbaya kuhusu nchi hiyo na kufanya

14:33 *Tnn., “ya ukahaba.” **14:34** *Au “ya kuwa maadui wangu.”

Waisraeli wote wamnung'uni-
kie Musa,^a **37** naam, wanau-
me hao walioleta habari mba-
ya kuhusu nchi hiyo wataua-
wa mbele za Yehova.^b **38** La-
kini Yoshua mwana wa Nuni
na Kalebui mwana wa Yefune,
waliokuwa miongoni mwa wa-
naume walioenda kuipelele-
za nchi, ndio watakaoendelea
kuishi.””^c

39 Musa alipowaambia Wa-
israeli wote maneno hayo,
watu walianza kuombole-
za kwa uchungu mwingi.
40 Hata waliamka asubuhi na
mapema na kujaribu kupanda
juu mlimani, wakisema: “Tuko
tayari kupanda mpaka mahali
ambapo Yehova alituambia,
kwa maana tumetenda dha-
mbi.”^d **41** Lakini Musa aka-
waambia: “Kwa nini mnakiu-
ka agizo la Yehova? Hamta-
fanikiwa. **42** Msipande kwenda
huko, kwa sababu Yehova
hayuko pamoja nanyi; mtashi-
ndwa na maadui wenu.”^e
43 Kwa maana Waamaleki na
Wakanaani watakabiliana na-
nyii huko,^f nao watawaanga-
miza kwa upanga. Kwa saba-
bu mliacha kumfuata Yehova,
Yehova hatakuwa pamoja
nanyi.”^g

44 Hata hivyo, kwa kimbe-
lembele wakapanda kuele-
kea mlimani,^h lakini sandu-
ku la agano la Yehova liliba-
ki katikati ya kambi, na Musa
pia alibaki.ⁱ **45** Ndipo Waa-
maleki na Wakanaani walioi-
shii kwenye mlima huo wa-
kashuka na kuanza kuwasham-
bulia, wakawatawanya mpa-
ka Horma.^j

15 Yehova akaendelea
kumwambia Musa:
2 “Wambie hivi Waisraeli:
‘Hatimaye mtakapoingia kati-

SURA YA 14

a Hes 13:32

b 1Ko 10:6,10
Yud 5c Hes 14:30
Hes 26:65
Hes 32:11,12
Kum 1:35,36
Yos 14:6

d Kum 1:41

e Law 26:14,17
Kum 1:42

f Hes 13:29

g 2Nya 15:2

h Kum 1:43

i Hes 10:33

j Hes 21:1,3
Kum 1:44

Safu ya 2

SURA YA 15

a Mwa 15:18

b Law 1:2,3

c Law 7:16
Law 22:18,19
Law 22:21d Law 23:4
Hes 28:16
Hes 29:1
Kum 16:13,16

e Law 1:9

f Kut 29:40
Law 2:1,11g Hes 28:6,7
Hes 28:11,14

h Law 1:3

i Law 7:16

j Law 3:1,3
Law 7:11

ka nchi ninayowapa mwi-
shi ndani yake,^a **3** na kumto-
lea Yehova dhabihu inayocho-
mwa kwa moto kutoka kati ya
mifugo au kundi—iwe ni dha-
bihu ya kuteketewa^b au dha-
bihu ya kutimiza nadhiri
ya pekee au toleo la hiari^c au
dhabihu mnayotoa wakati wa
sherehe zenu za majira,^d ili
kumtolea Yehova harufu in-
ayompendeza*^e— **4** ni lazima
pia mtu anayetoa dhabihu
yake amtotee Yehova sehemu
ya kumi ya kipimo cha efa
moja* ya unga laini^f uliocha-
nganywa na robo ya hini^g ya
mafuta ili iwe toleo la nafaka.
5 Pia mnapaswa kutoa robo
ya kipimo cha hini ya divai
ili iwe toleo la kinywaji; mtai-
toa pamoja na dhabihu ya ku-
teketezwa^g au pamoja na dha-
bihu ya kila mwanakondoo
dume. **6** Au mtatoa kondoo
dume pamoja na sehemu mbi-
li za kumi za kipimo cha efa
moja ya unga laini uliocha-
nganywa na sehemu ya tatu
ya hini ya mafuta kwa aji-
li ya toleo la nafaka. **7** Na-
nyii mnapaswa kutoa sehemu
ya tatu ya hini ya divai ili iwe
toleo la kinywaji lenye harufu
inayompendeza* Yehova.

8 “Lakini mkimtolea Yeho-
va mnyama dume kutoka kati-
ka mifugo yenu ili awe dhabi-
hu ya kuteketewa^h au dhabi-
hu ya kutimiza nadhiri ya pe-
keeⁱ au dhabihu za ushirika,^j
9 mnapaswa kumtoa mnya-
ma dume huyo pamoja na se-
hemu tatu za kumi za kipi-
mo cha efa moja ya unga lai-

15:3, 7 *Au “inayomtuliza.” **15:4** *Se-
hemu ya kumi ya efa ilikuwa sawa na lita
2.2 au kilogramu 1.3 hivi. Angalia Nyo-
ngeza B14. [#]Hini ilikuwa sawa na lita
3.67. Angalia Nyongeza B14.

ni uliochanganywa na nusu ya hini ya mafuta kwa ajili ya toleo la nafaka.^a **10** Mnapaswa pia kutoa nusu ya hini ya divai ili iwe toleo la kinywaji^b linalochomwa kwa moto lenye harufu inayompendeza* Yehova. **11** Hivyo ndivyo mnavyopaswa kumtoa kila ng'ombe dume au kila kondoo dume au kila mwanakondoo dume au mbuzi dume. **12** Haidhuru mnatoa wanyama wangapi, mnapaswa kutoa vitu hivyo pamoja na kila mnyama mnavyemtoa, kulingana na idadi yao. **13** Hivyo ndivyo kila Mwisraeli mwenyeji anavyopaswa kutoa dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.

14 “Ikiwa mgeni anayeishi nanyi au mtu mwingine ambaye ameishi pamoja nanyi kwa muda mrefu atatoa pia dhabihu ya kuteketewa yenye harufu inayompendeza* Yehova, anapaswa kufanya kama mnavyofanya.^c **15** Ninyi pamoja na mgeni anayeishi miongoni mweni mtafuata sheria zilezile. Itakuwa amri ya kudumu katika vizazi vyenu vyote. Ninyi pamoja na mgeni mtakuwa sawa mbele za Yehova.^d **16** Ninyi na mgeni anayeishi miongoni mweni mtafuata sheria zilezile na amri zilezile.”*

17 Yehova akaendelea kumwambia Musa, **18** “Wambie hivi Waisraeli: ‘Mtaka poingia katika nchi ninayowapeleka **19** nanyi mle chakula chochote cha* nchi hiyo,^e

15:10, 13, 14, 24 *Au “inayomtuli-za.” 15:16 *Tnn., “maamuzi yaleyale ya hukumu.” 15:19 *Tnn., “mkate wowote wa.”

SURA YA 15

a Law 6:14
Hes 28:11, 12
Hes 29:6

b Hes 28:11, 14

c Kut 12:49
Law 24:22
Hes 9:14

d Law 19:34

e Yos 5:11, 12

Safu ya 2

a Kut 23:19
Law 2:14
Hes 18:8, 12
Kum 26:1, 2
Met 3:9

b Hes 15:8-10

c Hes 28:15

d Law 4:20
Ebr 2:17
1Yo 2:1, 2

mnapaswa kumtolea Yehova kiasi fulani kama mchango. **20** Mtoa mchango wa mazao ya kwanza^a ya mikate ya mviringo iliyoowa kwa unga wenu ambao haujakobolewa. Mtaotoa kama mchango unaotoka katika uwanja wa kupuria nafaka. **21** Baadhi ya mazao ya kwanza ya unga wenu ambao haujakobolewa mtamtolea Yehova mchango katika vizazi vyenu vyote.

22 “Sasa mkifanya kosa, nanyi mkose kushika amri hizi zote ambazo mimi, Yehova, nimempa Musa, **23** mambo yote ambayo mimi, Yehova, nimewaamuru ninyi kupitia Musa katika vizazi vyenu tangu siku ambayo mimi Yehova niliamuru, **24** na ikiwa kosa hilo lilifanywa bila kuku- sudia na bila kusanyiko lote kujua, basi ni lazima kusanyiko lote litoe dhabihu ya kuteketewa ya ng'ombe dume mchanga ili iwe harufu inayompendeza* Yehova, pamoja na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji kulingana na utaratibu wa kawaida,^b na pia mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi.^c **25** Kuhani atatoa dhabihu ya kufunika dhambi ya kusanyiko lote la Waisraeli, nao watasamehewa,^d kwa sababu lilikuwa kosa, nao walimlelea Yehova dhabihu inayochomwa kwa moto na kuleta dhabihu yao ya dhambi mbele za Yehova kwa ajili ya kosa lao. **26** Kusanyiko lote la Waisraeli pamoja na wageni wanaokaa miongoni mwao watasamehewa kosa hilo kwa sababu watu wote walihusika.

27 “Mtu yeyote akifanya dhambi bila kuku- sudia,

ataoa mbuzi jike wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhambi ya dhambi.^a **28** Kisha kuhani ataoa dhambi ili mtu aliyetenda dhambi mbele za Yehova bila kukusudia asamehewe dhambi yake, yaani, atamtolea dhambi ya kufunika dhambi yake, na mtu huyo atasamehewa.^b **29** Waisraeli wenyeji na pia wageni wanaoishi miongoni mwao watafuata sheria zilezile zinazomhusu mtu anayetenda kosa bila kukusudia.^c

30 “Lakini mtu anayetenda kosa kimakusudi,^d awe ni mwenyeji au mgeni, anamkufuru Yehova, naye lazima auawe. **31** Kwa kuwa amedharau neno la Yehova na kuvunja amri yake, ni lazima mtu huyo auawe.^e Ataadhibiwa kwa sababu ya kosa lake.”^{*f}

32 Waisraeli walipokuwa nyikani, walimkuta mtu fulani akiokota kuni siku ya Sabato.^g **33** Wale waliomkuta akikusanya kuni wakamleta kwa Musa na Haruni na Waisraeli wote. **34** Wakamtia kifungoni^h kwa sababu sheria haikusema waziwazi mtu huyo afaanyiwe nini.

35 Basi Yehova akamwambia Musa: “Ni lazima mtu huyo auawe,ⁱ Waisraeli wote watampiga mawe nje ya kambi.”^j **36** Basi Waisraeli wote wakamtoa nje ya kambi, wakampiga mawe na kumuua, kama Yehova alivyomwamuru Musa.

37 Yehova akaendelea kumwambia Musa: **38** “Waabie Waisraeli wajitengenezee upindo wa nyuzinyuzi kwenye ncha za mavazi yao katika vizazi vyao vyote, nao wa-

15:31 * Tnn., “Kosa lake litakuwa juu ya kichwa chake.”

SURA YA 15

a Law 4:27, 28

b Law 4:32, 35

c Kut 12:49

Law 24:22

Hes 9:14

Hes 15:15

d Kut 21:14

Kum 17:12

Ebr 10:26, 27

e Ebr 10:28

f Eze 18:20

g Kut 20:9, 10

Kut 35:2

Kum 5:13, 14

h Law 24:11, 12

i Kut 31:14

j Law 24:14

Safu ya 2

a Kum 22:12

Mt 23:5

b Kum 11:18

c Kut 34:15

d Law 11:44

Ro 12:1

1Pe 1:15

e Mwa 17:8

Kut 29:45

Law 25:38

f Kut 3:15

Kut 6:2, 3

SURA YA 16

g Yud 11

h Kut 6:21

i Kut 6:18

j Kut 6:16

k Hes 26:7-9

l Mwa 46:8

m Hes 12:1, 2

Hes 14:2

Zb 106:16

n Kut 19:6

o Kut 29:45

p 2Ti 2:19

q Kut 28:43

Law 21:6

r Kut 28:1

Hes 17:5

Zb 105:26

s Hes 16:2

tashona uzi wa bluu juu ya upindo huo wa nyuzinyuzi.^a

39 ‘Mnapaswa kutengeneza upindo huo wa nyuzinyuzi ili muuone na kukumbuka amri zote za Yehova na kuzishika.^b Msifuute mioyo yenu na macho yenu, ambayo yanawangoza kwenye ukahaba wa ki-roho.^c **40** Upindo huo utawasaidia kukumbuka, nanyi mta-shika amri zangu zote na kuwa watakatifu kwangu mimi Mungu wenu.^d **41** Mimi ni Yehova Mungu wenu, niliyewatoa nchini Misri ili nijithibitisha kuwa Mungu wenu.^e Mimi ni Yehova Mungu wenu.”^f

16 Kisha Kora^g mwana wa Ishari,^h mwana wa Kohathi,ⁱ mwana wa Lawi,^j akau-ngana na Dathani na Abiramu wana wa Eliabu,^k na Oni mwana wa Pelethi, wazao wa Rubeni.^l **2** Nao, pamoja na wanaume 250 Waisraeli, wakuu wa kusanyiko, wanau-me maarufu waliowekwa rasmi wakaanza kumpinga Musa. **3** Basi wakakusanyika dhidi ya^m Musa na Haruni na kuwaambia: “Mmetuchosha! Kusanyiko lote ni takatifu,ⁿ watu wote, na Yehova yuko miongoni mwao.^o Basi, kwa nini mna-jikweza juu ya kutaniko la Yehova?”

4 Musa aliposikia jambo hilo, mara moja akaanguka chini kifudifudi. **5** Kisha akamwambia Kora na watu wote waliomuunga mkono, “Asubuhi Yehova ataonyesha ni nani aliye wake^p na ni nani aliye mtakatifu na ni nani anayepaswa kumkaribia,^q na yote atakayemchagua^r ndiye atakayemkaribia. **6** Fanyeni hivi: Wewe Kora na wote wanaokuunga mkono,^s chukue-

ni vyetezo,^a **7** kesho weke ni moto ndani yake na kutia uvumba juu yake mbele za Yehova, na mtu ambaye Yehova atamchagua,^b ndiye mtakatifu. Ninyi wana wa Lawi^c mmevuka mpaka!”

8 Kisha Musa akamwambia Kora: “Sikilizeni, tafadhali, ninyi wana wa Lawi. **9** Je, mnaona ni jambo dogo sana kwenu kwamba Mungu wa Israeli amewateua ninyi miongoni mwa Waisraeli^d wote na kuwaruhusu mumkaribie ili kutumikia katika hema la Yehova la ibada na kusimama mbele ya Waisraeli wote ili kuwahudumia,^e **10** na kuwaleta karibu naye ninyi pamoja na ndugu zenu wote, wana wa Lawi? Je, ni lazima pia mjaribu kunyakua ukuhani?^f **11** Kwa sababu hiyo, wewe na watu wote wanaokuunga mkono mnampinga Yehova. Haruni ni nani hivi kwamba mnung’unike kumhusu?”^g

12 Baadaye Musa akatuma ujumbe ili Dathani na Abiramu^h wana wa Eliabu waitwe, lakini wakasema: “Hatutakuja! **13** Je, unafikiri ni jambo dogo kututoa katika nchi inayotiririka maziwa na asali ili utuue nyikani?ⁱ Sasa, je, unataka kujifanya kiongozi mwenye mam-laka kamili juu yetu?”^j **14** Isitoshe, hujatuleta katika nchi yoyote inayotiririka maziwa na asali^k wala kutupatia urithi wa mashamba au shamba la mizabibu. Je, unataka kuto-boa macho ya watu hawa? Sisi hatutakuja!”

15 Basi Musa akakasirika sana na kumwambia Yehova: “Usikubali toleo lao la nafaka.

SURA YA 16

a Law 10:1

b Hes 3:10

c Hes 16:1

d Hes 3:9, 41

e Hes 1:53
Hes 3:6
Hes 4:4
Kum 10:8

f Flp 2:3

g Kut 16:8
Zb 106:16

h Hes 16:1

i Kut 16:3
Hes 14:28, 29j Kut 3:8
Law 20:24

Safu ya 2

a 1Sa 12:1, 3
Mdo 20:33
2Ko 7:2

b Hes 16:2

c Hes 12:5
Hes 14:10d Hes 3:10, 38
Hes 16:45e Ayu 12:10
Mhu 3:19
Mhu 12:7

f Mwa 18:23

g Hes 16:1, 2

h Hes 11:16

Sijachukua hata punda mmoja kutoka kwao, wala sijamdhuru mtu yeyote kati yao.”^a

16 Kisha Musa akamwambia Kora: “Kesho, fika mbele za Yehova, wewe pamoja na watu wote wanaokuunga mkono, wewe na watu hao pamoja na Haruni. **17** Kila mmoja wenu anapaswa kuchukua chetezo chake na kuweka uvumba juu yake, na kila mmoja atapeleka chetezo chake mbele za Yehova, vyetezo 250, pia wewe na Haruni mtapeleka kila mmoja chetezo chake.” **18** Basi kila mmoja wao akachukua chetezo chake, akaweka moto na uvumba juu yake na kusimama kwenye mlango wa hema la mkutano pamoja na Musa na Haruni. **19** Kora alipokuwa amewakusanya watu wote waliomuunga mkono^b kwenye mlango wa hema la mkutano ili kumpinga Musa na Haruni, utukufu wa Yehova ukawatokea watu wote waliokusanyika.^c

20 Kisha Yehova akamwambia Musa na Haruni, **21** “Jitengeni na kikundi hiki, ili nikiangamize mara moja.”^d **22** Ndipo Musa na Haruni wakaanguka chini kifudifudi na kusema: “Ee Mungu, Mungu wa roho ya watu wote,^e je, dhambi ya mtu mmoja ikufanye uwakasirikie watu wote waliokusanyika?”^f

23 Basi Yehova akamwambia Musa, **24** “Waambie hivi watu wote: ‘Ondokeni karibu na mahema ya Kora, Dathani, na Abiramu!’”^g

25 Kisha Musa akaondoka na kwenda kwa Dathani na Abiramu, na wazee^h wa

16:13 *Au “kupiga ubwana juu yetu.”

16:22 *Tnn., “roho za miili yote.”

Israeli wakaenda pamoja naye. **26** Musa akawaambia hivi watu wote: “Tafadhali, ondokeni karibu na mahema ya watu hawa waovu wala msiguse kitu chochote ambacho ni mali yao, msije mkafagiliwa mbali kwa sababu ya dhambi yao yote.” **27** Mara moja wakaondoka karibu na mahema ya Kora, Dathani, na Abiramu, wakaondoka kila upande, kisha Dathani na Abiramu wakatoka nje, wakasimama kwenye mlango wa mahema yao pamoja na wake zao, wana wao, na watoto wao wachanga.

28 Halafu Musa akasema: “Hivi ndivyo mtakavyojua kwamba Yehova amenituma nifanye mambo haya yote, na kwamba sijayatunga moyoni mwangu.* **29** Watu hawa wakifa kama wanavyokufa wanadamu wengine wote na kuadhibiwa kama wanadamu wengine wote, basi Yehova hajanituma.^a **30** Lakini Yehova akiwatendea jambo lili la kawaida, ardhi ifunguke* na kuwameza watu hawa pamoja na vitu vyao vyote, nao waingie Kaburini[#] wakiwa hai, mtajua kwa hakika kwamba wamemdharau Yehova.”

31 Mara tu alipomaliza ku-sema maneno hayo yote, ardhi ikafunguka chini yao.^b **32** Naam, dunia ikafunguka* na kuwameza watu hao pamoja na familia zao na watu wote wa Kora^c na mali zao zote. **33** Kwa hiyo watu hao pamoja na watu wao wote wakaingia

16:28 *Au “si matakwa yangu mwenyewe.” 16:30 *Tnn., “ifungue kinywa chake.” 16:30, 33 #Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 16:32 *Tnn., “ikafungua kinywa chake.”

SURA YA 16

a Kum 18:21, 22

b Hes 26:10
Kum 11:6
Zb 106:17c Kut 6:24
Hes 26:11
1Nya 6:31, 37

Safu ya 2

a Yud 11

b Law 10:1, 2
Hes 11:1c Hes 16:17
Hes 26:10
Zb 106:18

d Hes 16:6, 7

e Kut 38:1

f Hes 16:5
Hes 17:10g Hes 3:10
Hes 18:7
2Nya 26:16-18h Zb 106:17
Yud 11

i Hes 14:2

Kaburini[#] wakiwa hai, dunia ikawafunika, nao wakaangamia kutoka kati ya kutaniko.^a

34 Waisraeli wote waliokuwa wamewazunguka waliposikia vilio vyao wakakimbia wakisema: “Tunaogopa dunia itatumeza!” **35** Kisha moto ukashuka kutoka kwa Yehova^b na kuwateketeza wale wanaume 250 waliokuwa wakifukiza uvumba.^c

36 Kisha Yehova akamwambia Musa, **37** “Mwambie Eleazari mwana wa kuhani Haruni achukue vyetezo^d hivyo kutoka motoni kwa sababu ni vitakatifu. Mwambie pia autawanye moto huo mbali kidogo na mahali hapo. **38** Vyetezo vya wanaume waliouawa kwa sababu ya dhambi yao vinapaswa kunyoosha ili viwe mabamba membamba ya kufunika madhabahu,^e kwa sababu walivipeleka mbele za Yehova, navyo vikawa vitakatifu. Vinapaswa kuwa onyo kwa Waisraeli.”^f **39** Basi kuhani Eleazari akachukua vyetezo vya shaba vilivyoletwa na wale wanaume waliokuwa wametekelezwa, akavipiga na kuvinyoosha ili vifunike madhabahu, **40** kama Yehova alivyomwambia kupitia Musa. Viliwakumbusha Waisraeli kwamba mtu yeyote asiye na idhini* ambaye si mzao wa Haruni hapaswi kukaribia madhabahu ili kumfukizia Yehova^g uvumba na kwamba mtu yeyote asiwe kama Kora na wale waliomuunga mkono.^h

41 Siku iliyofuata, kusanyi-ko lote la Waisraeli likianza kumnung'unikia Musa na Haruni,ⁱ likisema: “Ninyi wawi-

16:40 *Tnn., “mgeni yeyote.”

li mmewaua watu wa Yehova.” **42** Watu wote walipokuwa wamekusanyika dhidi ya Musa na Haruni, waligeuka kuelekea hema la mkutano, na tazama! wingu lifufunika hema hilo, na utukufu wa Yehova ukaanza kuonekana.^a

43 Musa na Haruni wakaeenda mbele ya hema la mkutano,^b **44** na Yehova akamwambia Musa, **45** “Ninyi wanaume, jitengeni na kusanyiko hili ili niliangamize mara moja.”^c Ndipo Musa na Haruni wakaanguka chini kifufufu.^d **46** Kisha Musa akamwambia Haruni, “Chukua chetezo uweke moto ndani yake kutoka katika madhabahu^e na uweke uvumba juu yake, nawe uende haraka kwao na kuu-fukiza ili dhambi yao ifunike,^f kwa sababu Yehova amekasirika. Pigo limeanza!” **47** Mara moja Haruni akachukua chetezo, kama Musa alivyomwambia, akakimbia katikati ya kusanyiko hilo, na pigo lilikuwa limeanza kuwaathiri watu. Basi akaweka uvumba juu ya chetezo, akaanza kuu-fukiza ili dhambi yao ifunike. **48** Akaendelea kusimama katikati ya watu waliokufa na walio hai, hatimaye pigo hilo likaisha. **49** Watu walio-kufa kutokana na pigo hilo walikuwa 14,700, bila kuwahesabu wale waliokufa kwa sababu ya Kora. **50** Mwishowe Haruni aliporudi kwa Musa kwenye mlango wa hema la mkutano, pigo hilo lilikuwa limekomeshwa.

17 Kisha Yehova akamwambia Musa, **2** “Zungumza na Waisraeli na uchu-kue kutoka kwao fimbo moja kwa ajili ya kila kabila, kuto-

SURA YA 16

a Kut 16:7
Hes 14:10
Hes 16:19

b Hes 20:2, 6

c Kut 23:20, 21
1Ko 10:6, 10

d Hes 16:21, 22

e Law 6:12

f Kut 34:9
Hes 8:19

Safu ya 2

SURA YA 17

a Hes 1:4, 16

b Kut 34:29

c Kut 25:22
Kut 30:36
Law 16:2

d Hes 16:5

e Hes 11:1
Hes 14:27
Hes 16:11
1Ko 10:6, 10

f Hes 14:2
Hes 16:13, 41

g Ebr 9:4

h Hes 16:38

i Kum 9:7
Kum 31:27

ka kwa wakuu wa kila kabila,^a jumla ya fimbo 12. Andika jina la kila mmoja wao kwenye fimbo yake. **3** Unapaswa kuandika jina la Haruni kwenye fimbo ya Lawi, kwa sababu kuna fimbo moja kwa ajili ya kiongozi wa kila kabila. **4** Ziweke fimbo hizo ndani ya hema la mkutano mbele ya sanduku la Ushahidi,^b mahali ambapo mimi hukutokea kwa ukawaida.^c **5** Na fimbo ya mtu nitakayemchagua^d itachipua, nami nitakomesha manung'uniko ya Waisraeli dhidi yangu,^e ambayo pia wanakunung'unikia.”^f

6 Basi Musa akazungumza na Waisraeli, na wakuu wao wote wakampa fimbo—fimbo moja kutoka kwa kila mkuu wa kabila, fimbo 12—nayo fimbo ya Haruni ilikuwa kati ya fimbo zao. **7** Kisha Musa akaziweka fimbo hizo mbele za Yehova katika hema la Ushahidi.

8 Siku iliyofuata, Musa ali-poingia katika hema la Ushahidi, aliona fimbo ya Haruni ya kabila la Lawi imetokeza matumba nayo ilikuwa ikichanua maua na kuzaa matunda ya lozi yaliyoiva. **9** Kisha Musa akazichukua fimbo zote kutoka mbele za Yehova na kuzileta mbele ya Waisraeli wote. Wakazitazama na kila mkuu akachukua fimbo yake.

10 Halafu Yehova akamwambia Musa, “Irudishe fimbo ya Haruni^g mbele ya sanduku la Ushahidi ili iwekwe kuwa onyo^h kwa wana wa kuasi,ⁱ ili manung'uniko yao dhidi yangu yakome na ili wasife.” **11** Mara moja Musa akafanya

kama Yehova alivyomwamuru. Hivyo ndivyo alivyofanya.

12 Kisha Waisraeli waka-mwambia Musa, “Sasa tutakufa, bila shaka tutaangamia, sisi sote tutaangamia! **13** Hata mtu yeyote atakayekaribia hema la Yehova la ibada atakufa!^a Je, ni lazima sote tufe kwa njia hiyo?”^b

18 Kisha Yehova akamwambia Haruni, “Wewe na wana wako na ukoo wako* mtawajibika ikiwa kosa lolote litafanywa dhidi ya mahali patakatifu,^c na wewe na wana wako lolote litafanywa dhidi ya ukuhani wenu.^d **2** Pia walete ndugu zako wa kabila la Lawi, kabila la mababu zako, ili wajiunge nawe na kukuhudumia wewe^e pamoja na wanao mbele ya hema la Ushahidi.^f **3** Wanapaswa kutimiza majukumu utakayowapa na utumishi wa hema lote.^g Hata hivyo, hawapaswi kukaribia vyombo vya mahali patakatifu na madhabahu, ili wewe pamoja nao msife.^h **4** Watajiunga nawe na kutimiza majukumu yao kuhusiana na hema la mkutano na utumishi wote katika hema hilo, na mtu yeyote asiye na idhini* hapaswi kuwakaribia ninyi.ⁱ **5** Ni lazima mtimize majukumu yenu ya mahali patakatifu/ na madhabahu,^k ili ghadhabu/ yangu isije tena juu ya Waisraeli. **6** Mimi mwenyewe nimewachukua ndugu zenu, Walawi, kutoka miongoni mwa Waisraeli na kuwakabidhi ninyi kama zawadi.^m Wamekabidhiwa kwa Yehova ili watu-

18:1 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. **18:4, 7** *Tnn., “mgeni yeyote,” yaani, mtu ambaye si wa familia ya Haruni.

SURA YA 17

a Hes 1:51
Hes 18:4, 7
b Hes 16:49

SURA YA 18

c Kut 25:8
Law 21:10-12
d Kut 28:38
Law 22:9
Hes 18:23
e Hes 3:6
Hes 8:22
Hes 16:9
f Hes 1:53
g Hes 3:25, 26
Hes 3:30, 31
Hes 3:36, 37
h Hes 4:15, 20
Hes 16:39, 40
i Hes 1:51
Hes 3:10
j Law 24:2, 3
Hes 3:32
k Kut 30:7
l Hes 16:46
m Hes 3:9, 12
Hes 8:15, 16

Safu ya 2

a Hes 8:19
b Law 16:2, 12
Ebr 9:3, 7
c 1Sa 2:28
Ebr 5:4
d Hes 3:10
Hes 16:39, 40
e Kut 23:19
Law 27:28, 30
Hes 18:11, 26
f Law 7:34
Hes 5:9
g Law 2:3
h Law 5:11, 12
Law 6:25, 26
i Law 7:1, 7
j Kut 29:32
Law 6:14, 16
Law 10:12, 13
k Law 6:18
Law 7:1, 6
Law 14:13
Law 21:22
l Hes 15:20
Eze 44:30
m Kut 29:27
Law 7:34
n Law 10:14
Kum 18:3
o Law 22:4-6
p Met 3:9
q Law 2:14
Kum 18:4

mikie katika hema la mkutano.^a **7** Wewe na wanao mna wajibu wa kufanya kazi za ukuhani zinazohusu madhabahu na vitu vilivyo nyuma ya pazia,^b nanyi mtatimiza utumishi huo.^c Nimewapa utumishi wa ukuhani kama zawadi, na mtu yeyote asiye na idhini* atakayekaribia mahali patakatifu anapaswa kuuawa.”^d

8 Yehova akaendelea ku-mwambia Haruni: “Mimi mwenyewe nilikuwika usimamie michango ninayoletewa.^e Nimekupa wewe na wanao sehemu ya vitu vyote vitakati-fu vinavyotolewa kama mchango na Waisraeli ili viwe posho yenu ya kudumu.^f **9** Hivi ndivyo vitakavyokuwa vitu vye-nu kutoka katika matoleo yote matakati-fu kabisa yanayocho-mwa kwa moto: matoleo yao yote, kutia ndani matoleo yao ya nafaka^g na dhabihu zao za dhambi^h na dhabihu zao za hatiaⁱ wanazoniletea. Ni vitu vitakati-fu kabisa kwako na wanao. **10** Mtavila vitu hivyo mahali patakatifu zaidi.^j Kila mwanamume anaweza kuvila. Vitakuwa vitu vitakati-fu kwe-nu.^k **11** Vitu hivi pia vitaku-wa vyenu: zawadi ambazo Waisraeli wanatoa kuwa mchango/ pamoja na matoleo yao yote ya kutikiswa.^m Nimekupa wewe na wanao na mabinti wako vitu hivyo ili viwe posho yenu ya kudumu.ⁿ Kila mtu aliy safi katika nyumba yako anaweza kula.^o

12 “Mafuta yote bora na di-vai yote mpya na nafaka, mazao yao ya kwanza,^p ambayo wanampa Yehova, ninakupa wewe.^q **13** Mazao yote ya kwanza yaliyokomaa ya ardhi yao, ambayo watamletea Ye-

hova, yatakuwa yako.^a Kila mtu aliye safi katika nyumba yako anaweza kula.

14 "Kila kitu kilichotolewa kwa ajili yangu* katika Israeli kinapaswa kuwa chako.^b

15 "Kila mzaliwa wa kwanza wa viumbe wote walio hai,^c ambaye watanitolea mimi Yehova, awe ni mwana-damu au mnyama, anapaswa kuwa wako. Hata hivyo, ni lazima uwakomboe wazaliwa wa kwanza wa wanadamu,^d na unapaswa pia kuwakomboa wazaliwa wa kwanza wa wanyama wasio safi.^e

16 Unapaswa kumkomboa mzaliwa wa kwanza kwa bei ya ukombozi akiwa na umri wa kuanzia mwezi mmoja na zaidi, kwa thamani iliyokadiriwa ya shekeli tano za fedha,^{*f} kulingana na shekeli ya kawaida ya mahali patakatifu.[#] Ni gera 20.[^] **17** Lakini hupaswi kumkomboa^g ng'ombe dume ambaye ni mzaliwa wa kwanza au mwanakondoo dume ambaye ni mzaliwa wa kwanza au mbuzi ambaye ni mzaliwa wa kwanza. Hao ni watakatifu. Unapaswa kunyunyiza damu yao kwenye madhabahu,^h na mafuta yao unapaswa kuyateketeza ili yafuke moshi yakiwa dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.ⁱ **18** Nyama yao itakuwa yako. Itakuwa yako sawa na kidari cha to-

18:14 *Yaani, kila kitu kilichofanywa kuwa kitakatifu kwa Mungu kwa kuwa hakiwezi kukombolewa au kuchukuliwa tena. **18:16** *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. [#]Au "shekeli takatifu." [^]Gera moja ilikuwa na uzito wa gramu 0.57. Angalia Nyongeza B14. **18:17** *Au "inayomtuliza."

SURA YA 18

a Kut 23:19

b Law 27:21, 28

c Kut 13:2
Law 27:26
Hes 3:13

d Kut 13:13

e Kut 34:20
Law 27:27

f Law 27:6

g Kut 22:30
Kum 15:19

h Law 17:11

i Law 3:16

Safu ya 2

a Kut 29:26
Law 7:31, 34b Kut 23:19
Hes 15:18, 19
Hes 18:11, 26
Hes 31:28, 29

c 2Nya 31:4

d Hes 26:62, 63
Kum 10:9
Kum 14:27
Yos 14:3e Kum 18:1, 2
Yos 18:7
Eze 44:28f Law 27:30
Ne 10:37
Ne 12:44
Ebr 7:5g Hes 3:6, 7
Hes 18:1

h Yos 13:33

i Kum 10:9

j Hes 18:21
Kum 12:19

leo la kutikiswa na mguu wa kulia.^a **19** Michango yote mitakatifu ambayo Waisraeli wataamkia Yehova,^b nimekuwa wewe na wanao na mabinti wako, ili iwe posho yenu ya kudumu.^c Ni agano la chumvi linalodumu* mbele za Yehova kwa ajili yako na wazao wako."

20 Yehova akaendelea kumwambia Haruni: "Hutakuwa na urithi katika nchi yao, wala hutakuwa na sehemu ya* ardhi miongoni mwao.^d Mimi ni fungu lako na urithi wako miongoni mwa Waisraeli.^e

21 "Ona kwamba nimewapa wana wa Lawi kila sehemu ya kumi^f katika Israeli iwe urithi wao kwa sababu ya utumishi wao, utumishi wa hema la mkutano. **22** Waisraeli wasikaribie tena hema la mkutano ili wasitende dhambi na kufa. **23** Ni Walawi tu watakotumikia katika hema la mkutano, na ndio watakoawajibika kwa ajili ya makosa yao.^g Ni sheria ya kudumu katika vyuzi vyenu kwamba hawapaswi kuchukua urithi miongoni mwa Waisraeli.^h **24** Kwa maana nimewapa Walawi sehemu ya kumi ambayo Waisraeli wanaitolea mchango, mimi Yehova, ili iwe urithi wao. Ndiyo sababu nimewaaambia, 'Hawapaswi kuchukua urithi miongoni mwa Waisraeli.'"ⁱ

25 Kisha Yehova akamwambia Musa, **26** "Unapaswa kuwaambia hivi Walawi: 'Mtapokea kutoka kwa Waisraeli sehemu ya kumi ambayo nimewapa ninyi kutoka kwao ili iwe urithi wenu,^j nanyi

18:19 *Yaani, agano linalodumu na lisi-lobadilika. **18:20** *Au "fungu la."

mnapaswa kumtolea Yehova mchango wa sehemu ya kumi kutoka katika sehemu hiyo ya kumi.^a **27** Sehemu hiyo itahesabiwa kuwa mchango wenu, itaonwa kama nafaka kutoka katika uwanja wa kupuria^b au divai yote inayotoka katika shinikizo la divai au mafuta yote yanayotoka katika shinikizo la mafuta. **28** Kwa njia hiyo mtamtolea Yehova mchango kutoka katika sehemu zote za kumi mnazopokea kutoka kwa Waisraeli, na kutoka kwa sehemu hizo mnapaswa kumtolea Yehova mchango na kumpa kuhani Haruni. **29** Mtamtolea Yehova mchango yote kutoka katika zawadi bora zaidi mnazopokea,^c ambazo ni takatifu.’

30 “Nawe unapaswa kuwaambia, ‘Mnapotoa vitu bora zaidi kutoka katika zawadi hizo kuwa mchango, mchango huo wa Walawi utaoonwa kama nafaka kutoka katika uwanja wa kupuria na kama divai inayotoka katika shinikizo la divai au mafuta yanayotoka katika shinikizo la mafuta. **31** Ninyi na familia zenu mna-weza kula vitu hivyo mahali popote kwa sababu ni malipo kwa ajili ya utumishi wenu katika hema la mkutano.^d **32** Hamtakuwa na hatia ya dhambi maadamu mnaitolea vitu bora kutoka katika zawadi hizo, nanyi hampaswi kuchafua vitu vitakatifu vya Waisraeli, msije mkafa.”^e

19 Yehova akamwambia tena Musa na Haruni, **2** “Hii ndiyo sheria ambayo mimi Yehova nimeamuru, ‘Waambieni Waisraeli wawaletee ng’ombe mwekundu amba-

SURA YA 18

a Ne 10:38

b Hes 15:20

c Hes 18:8, 12

d 1Ko 9:13

e Law 22:2, 15

Safu ya 2

SURA YA 19

a Law 22:20
Mal 1:14

b Ebr 9:13, 14

c Law 4:11, 12

d Zb 51:7

e Ebr 9:13, 14

f Hes 19:13, 21

g Kut 12:49
Law 24:22
Hes 15:15

ye hana kasoro yoyote^a na ambaye hajawahi kufungwa nira. **3** Mtampa kuhani Eleazari ng’ombe huyo, naye atampeleka nje ya kambi na kuchinjwa mbele yake. **4** Kisha kuhani Eleazari atachukua kwa kidole chake kiasi kidogo cha damu ya ng’ombe huyo na kuinyunyiza mara saba kuelekea upande wa mbele wa hema la mkutano.^b **5** Kisha ng’ombe huyo atateketezwa mbele ya macho yake. Ngozi yake na nyama yake na damu yake pamoja na mavi yake yateketezwa.^c **6** Halafu kuhani atachukua tawi la mwe-rezi, tawi la hisopo,^d na kitambaa chekundu na kutupa vitu hivyo katika moto unao-mteketeza ng’ombe huyo. **7** Kisha kuhani atafua mavazi yake na kuoga kwenye maji, halafu anaweza kurudi kambini; lakini kuhani huyo hatakuwa safi mpaka jioni.

8 “Mtu aliyemteketeza ng’ombe huyo atafua mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye hatakuwa safi mpaka jioni.

9 “Mtu aliye safi atayakusanya majivu ya ng’ombe huyo^e na kuyapeleka mahali safi nje ya kambi, yatahifadhiwa na Waisraeli ili yatumiwe kutengeneza maji ya kutakasa.^f Ni dhabihu ya dhambi. **10** Yule anayekusanya majivu ya ng’ombe huyo atafua mavazi yake, na hatakuwa safi mpaka jioni.

“Hiyo itakuwa sheria ya kudumu kwa Waisraeli na wageni wanaoishi miongoni mwao.^g

11 Mtu yeyote anayemgusa mtu aliyekufa* hatakuwa safi

19:11 *Au “nafsi iliyokufa ya mwanadamu yeyote.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

kwa siku saba.^a **12** Mtu huyo anapaswa kujitakasa kwa maji hayo siku ya tatu, na siku ya saba atakuwa safi. Lakini asi-pojitakasa siku ya tatu, hatakuwa safi siku ya saba. **13** Mtu yeyote anayemgusa mtu aliyekufa lakini hajatakasi amechafua hema la Yehova la ibada,^b na ni lazima mtu huyo auawe kutoka katika Israeli.^c Kwa sababu hajanyunyiziwa maji ya kutakasa,^d ataendelea kuwa mchafu. Yeye bado ni mchafu.

14 “Hii ndiyo sheria kuhusu mtu anayefia ndani ya hema: Kila mtu anayeingia katika hema hilo na kila mtu aliyekuwa ndani ya hema hilo wakati huo, hatakuwa safi kwa siku saba.

15 Kila chombo kilichofunuliwa ambacho kifuniko chake hakijafungwa kwa kamba si safi.^e **16** Kila mtu aliyeye uwanjani anayemgusa mtu aliyeuawa kwa upanga au maiti au mfupa wa mtu au kaburi hatakuwa safi kwa siku saba.^f

17 Kwa ajili ya mtu huyo asiye safi, watachukua majivu ya dhabihu ya dhambi iliyotekezwa na kuyamiminia maji ya kijito katika chombo. **18** Kisha mtu aliyeye safi^g atachukua tawi la hisopo^h na kulichovya ndani ya maji hayo na kunyunyizia hema na vyombo vyote na watu waliokuwa ndani ya hema hilo na mtu aliyegusa mfupa au mtu aliyeuawa au maiti au kaburi. **19** Siku ya tatu na siku ya saba, mtu aliyeye safi atamnyunyizia maji hayo mtu asiye safi na kumtakasa dhambi yake siku ya saba;ⁱ kisha atafua mavazi yake na kuoga kwenye maji, naye atakuwa safi jioni.

SURA YA 19

a Law 21:1, 11
Hes 5:2
Hes 6:9
Hes 9:6
Hes 31:19

b Law 15:31

c Law 22:3
Ebr 10:28

d Hes 19:9

e Law 11:31, 32

f Hes 19:11
Hes 31:19

g Hes 19:9

h Zb 51:7

i Law 14:9
Hes 19:12
Hes 31:19

Safu ya 2

a Hes 19:13

b Hes 19:18
Ebr 9:9, 10
Ebr 9:13, 14

c Law 15:4, 5

SURA YA 20

d Hes 13:26
Hes 20:22
Hes 33:36
Kum 2:14

e Kut 15:20
Hes 26:59
Mik 6:4

f Kut 17:1

g Kut 17:2

h Kut 14:11
Kut 17:3
Hes 16:13, 14
Hes 21:5

i Kum 8:14, 15

j Kum 8:7, 8

k Kut 16:10
Hes 14:10

20 “Lakini mtu asiye safi ambaye hatajitakasa ni lazima auawe kutoka kutanikoni^a kwa sababu amechafua mahali patakatifu pa Yehova. Kwa kuwa hakunyunyiziwa maji ya kutakasa, yeye si safi.

21 “Hii itakuwa sheria ya kudumu kwa ajili yao: Yule anayenyunyiza maji ya kutakasa^b anapaswa kufua mavazi yake, na yule anayegusa maji ya kutakasa hatakuwa safi mpaka jioni. **22** Kitu chochote kinachoguswa na mtu asiye safi hakitakuwa safi, na mtu anayekigusa hatakuwa safi mpaka jioni.”^c

20 Katika mwezi wa kwanza, Waisraeli wote walifika katika nyika ya Zini, wakaanza kukaa Kadeshi.^d Miriamu^e akafa na kuzikwa huko.

2 Mahali hapo hapakuwa na maji kwa ajili ya Waisraeli,^f basi wakakusanyika dhidi ya Musa na Haruni. **3** Watu wakagombana na Musa^g wakisema: “Laiti tungekufa ndugu zetu walipokufa mbele za Yehova! **4** Kwa nini mmelileta kutaniko la Yehova katika nyika hii ili sisi na mifugo yetu tufie humu?”^h **5** Na kwa nini mlitotoa Misri na kutoleta mahali hapa paovu?ⁱ Huku hakuna mbegu na tini na mizabibu na makomamanga, wala hakuna maji ya kunywa.”^j **6** Basi Musa na Haruni wakatoka mbele yao na kwenda kwenye mlango wa hema la mkutano, wakaanguka chini kifudifudi, na utukufu wa Yehova ukaanza kuwatokea.^k

7 Kisha Yehova akamwambia Musa, **8** “Ichukue ile fimbia, kisha wewe na Haruni ndugu yako muwakusanye

watu wote, halafu uzungumze na mwamba mbele ya macho yao ili utoe maji, nawe utatoa maji katika mwamba huo na kuwapa watu wote pamoja na mifugo yao maji ya kunywa.”^a

9 Kwa hiyo, Musa akachukua fimbo kutoka mbele za Yehova,^b kama Alivyomwamuru.

10 Basi Musa na Haruni wakawakusanya watu wote mbele ya mwamba huo, akawaambia, “Sikilizeni sasa, enyi waasi! Je, ni lazima tuwatolee maji katika mwamba huu?”^c

11 Ndipo Musa akainua mkono wake na kuupiga mwamba huo mara mbili kwa fimbo yake, na maji mengi yakaaanza kububujika, watu wakaaanza kunywa pamoja na mifugo yao.^d

12 Baadaye Yehova akamwambia hivi Musa na Haruni: “Kwa sababu hamkuonyesha kwamba mna imani kwangu na kunitakasa mbele ya Waisraeli, hamtawaingiza watu hawa katika nchi ambayo nitawapa.”^e **13** Hayo ndiyo maji ya Meriba,^{*f} mahali ambapo Waisraeli waligombana na Yehova, naye akawathibitishia kwamba yeye ni mtaakatifu.

14 Kisha Musa akawatuma wajumbe kutoka Kadeshi ili waende kwa mfalme wa Edomu,^g wamwambie: “Ndugu yako Israeli^h anasema hivi: ‘Unajua vizuri matatizo yote tuliopata. **15** Baba zetu walienda Misri,ⁱ nasi tuliishi Misri kwa miaka mingi,^{*j} nao Wamisri walitutesa sisi na baba zetu.^k **16** Mwishowe tulimlilia Yehova,^l naye akasikia ki-

20:13 *Maana yake “Kugombana.”
20:15 *Tnn., “siku nyingi.”

SURA YA 20

a Kut 17:5, 6
Zb 78:15,
Zb 105:41
Zb 114:8
Isa 48:21

b Kut 7:12, 19
Hes 17:10

c Zb 106:32, 33

d 1Ko 10:1, 4

e Hes 27:12-14
Kum 1:37
Kum 3:26
Kum 32:51, 52
Kum 34:4
Yos 1:2

f Zb 106:32, 33

g Amu 11:17

h Mwa 36:8
Kum 2:4
Kum 23:7

i Mwa 46:6

j Mwa 15:13
Kut 12:40

k Kut 1:11, 14

l Kut 2:23
Kut 3:7

Safu ya 2

a Kut 14:19
Kut 23:20
Kut 33:2

b Hes 21:21, 22
Kum 2:26, 27

c Kum 2:5, 6

d Kum 2:26, 28

e Amu 11:17

f Kum 2:8
Amu 11:18

g Hes 21:4
Hes 33:37

h Hes 33:38
Kum 32:50

lio chetu na kumtuma malai-ka;^a akatutoa Misri, na sasa tuko hapa Kadeshi, jiji linalopakana na eneo lako. **17** Tafadhali turuhusu tupite katika nchi yako. Hatutapita katika mashamba yenu au shamba lolote la mizabibu, nasi hatutakunywa maji ya kisima chochote. Tutafuata Barabara ya Mfalme bila kugeka kulia au kushoto mpaka tutakapokuwa tumepita katika eneo lako.”^b

18 Hata hivyo, mfalme wa Edomu akamwambia, “Usipite katika eneo letu. Ukipita, nitatoka na kukushambulia kwa upanga.” **19** Basi Waisraeli wakamwambia, “Tutafuata barabara kuu, na ikiwa sisi na mifugo yetu tutakunywa maji yako, tutalipa.”^c Sisi tunataka tu kupita kwa miguu, hatutaki kitu kingine chochote.”^d **20** Lakini bado akasema, “Hamtapita.”^e Ndipo mfalme wa Edomu akatoka ili kumshambulia akiwa na watu wengi na jeshi lenye nguvu.^{*} **21** Basi mfalme wa Edomu akakataa kuwaruhusu Waisraeli wapite katika eneo lake; kwa hiyo Waisraeli wakageuka na kumwacha.^f

22 Waisraeli wote wakaoondoka Kadeshi na kufika kwenye Mlima Hori.^g **23** Kisha Yehova akamwambia hivi Musa na Haruni kwenye Mlima Hori karibu na mpaka wa nchi ya Edomu: **24** “Haruni atakufa na kuzikwa kama watu wake walivyozikwa.^{*h} Hataingia katika nchi nitakayowapa Waisraeli, kwa sababu ninyi wawili mliasi agi-

20:20 *Tnn., “mkono wenye nguvu.”
20:24 *Tnn., “atakusanywa kwa watu wake.” Huu ni msemo wa kishairi unao-rejelea kifo.

zo nililowapa kuhusu maji ya Meriba.^a **25** Mchukue Haruni na Eleazari mwanawe, uwalite juu kwenye Mlima Hori. **26** Mvue Haruni mavazi yake^b umvishe Eleazari^c mwanawe, kisha Haruni atafia huko.”*

27 Basi Musa akafanya kama Yehova alivyomwamuru, nao wakapanda Mlima Hori watu wote wakiwatazama. **28** Kisha Musa akamvua Haruni mavazi yake na kumvisha Eleazari mwanawe. Baada ya hayo, Haruni akafa juu ya mlima huo.^d Kisha Musa na Eleazari wakateremka kutoka mlimani. **29** Waisraeli wote walipoona kwamba Haruni amekufa, nyumba yote ya Israeli ikamwombolezea Haruni kwa siku 30.^e

21 Mfalme Mkanaani wa Aradi,^f aliyeshi Negebu, aliposikia kwamba Waisraeli walipitia njia ya Atharimu, aliwashambulia na kuwateka baadhi yao. **2** Kwa hiyo Waisraeli wakamwekea Yehova nadhiri hii: “Ukiwatia watu hawa mikononi mwetu, bila shaka tutayaangamiza majiji yao.” **3** Kwa hiyo Yehova akawasikiliza Waisraeli na kuwatia Wakanaani mikononi mwao, Waisraeli wakawaangamiza pamoja na majiji yao. Basi wakapaita mahali hapo Horma.^{*g}

4 Walipoendelea na safari yao kutoka Mlima Hori^h kupitia njia ya Bahari Nyekundu ili kuizunguka nchi ya Edomu,ⁱ watu wakachoshwa na safari. **5** Na watu wakaendelea kumnung'unikia Mungu

20:26 *Tnn., “atakusanywa na kufia huko.” 21:3 *Maana yake “Kuanga-miza.”

SURA YA 20

a Hes 20:12
Kum 32:51, 52

b Kut 28:2
Kut 29:29

c Kut 6:23
Hes 4:16

d Hes 33:39
Kum 10:6
Kum 32:50

e Kum 34:8

SURA YA 21

f Hes 33:40
Yos 12:7, 14

g Hes 14:45

h Hes 33:41

i Hes 20:21
Kum 2:8
Amu 11:18

Safu ya 2

a Kut 14:11
Kut 15:24
Hes 16:13

b Hes 20:5

c Kut 16:15
Hes 11:6
Zb 78:24, 25

d 1Ko 10:6, 9

e Zb 78:34

f Kut 32:11

g 2Fa 18:1, 4

h Yoh 3:14, 15

i Yoh 6:40

j Hes 33:43

k Hes 33:44

l Kum 2:13

m Hes 22:36
Amu 11:18

na Musa,^a wakisema: “Kwa nini mmetutoa Misri ili tufe nyikani? Hakuna chakula wala maji,^b nasi tumeuchukia mkate huu unaochukiza.”^c

6 Basi Yehova akaleta nyoka wenye sumu* katikati ya watu, na nyoka hao wakawau- ma sana hivi kwamba Waisraeli wengi wakafa.^d

7 Kwa hiyo watu wakaja kwa Musa na kumwambia: “Tumetenda dhambi kwa kumnung'unikia Yehova na wewe pia.^e Msihi Yehova atuondolee nyoka hawa.” Basi Musa akamsihi Mungu kwa niaba ya watu.^f **8** Kisha Yehova akamwambia Musa: “Tengeneza mfano wa nyoka mwenye sumu na uuweke juu ya nguzo. Mtu yeyote akiu- mwa na nyoka, ni lazima autazame mfano huo ili aendelee kuishi.” **9** Mara moja Musa akatengeneza nyoka wa shaba^g na kumweka juu ya nguzo,^h na mtu yeyote aliyemwa na nyoka na kumtazama nyoka huyo wa shaba, aliendelea kuishi.ⁱ

10 Kisha Waisraeli wakae- ndelea na safari na kupi- ga kambi Obothi.^j **11** Hala- fu wakaondoka Obothi na ku- piga kambi Iye-abarimu,^k ka- tika nyika inayoelekeana na Moabu, upande wa mashari- ki. **12** Kutoka huko wakasa- firi na kupiga kambi karibu na Bonde la Zeredi.^l **13** Wa- kaondoka huko na kupiga ka- mbi katika eneo la Arnoni,^m lililo katika nyika inayoanzia kwenye mpaka wa Waamori, kwa maana eneo la Arno- ni ni mpaka wa Moabu, kati ya Wamoabu na Waamori.

21:6 *Tnn., “wenye moto.”

14 Ndiyo sababu kitabu cha Vita vya Yehova kinasema kuhusu "Jiji la Vahebu katika eneo la Sufa na mabonde* ya Arnoni, **15** na miteremko ya mabonde, inayofika katika mji wa Ari na kufika kwenye mpaka wa Moabu."

16 Kisha wakasafiri mpaka Beeru. Ni kwenye kisima hicho ambapo Yehova alimwambia Musa hivi: "Wakusanye watu, niwape maji."

17 Wakati huo, Waisraeli waliimba wimbo huu:

"Bubujika, Ee kisima!
—Kiimbieni!"

18 Kisima kilichochimbwa na wakuu, kilichochimbwa na watu mashuhuri, Kwa fimbo ya kiongozi na kwa fimbo zao wenyewe."

Kisha watokoa nyikani na kwenda Matana, **19** kutoka Matana mpaka Nahalieli, na kutoka Nahalieli mpaka Bamothi.^a **20** Wakatoka Bamothi na kwenda kwenye bonde lililo katika eneo la Moabu,^b juu ya Pisga,^c linaloelekeana na Yeshimoni.^d

21 Sasa Waisraeli wakawatumia wajumbe wakamwambie hivi Sihoni mfalme wa Waamori:^e **22** "Turuhusu tupite katika nchi yako. Hatutageuka na kuingia katika mashamba yenu au shamba lolote la mizabibu. Hatutakunywa maji ya kisima chochote. Tutafuata Barabara ya Mfalme mpaka tutakapokuwa tumepita katika eneo lako."^f **23** Lakini Sihoni hakuwaruhusu Waisraeli

21:14 *Au "makorongo." 21:17 *Au "Kitikieni." 21:20 *Au labda, "jangwa; nyika."

SURA YA 21

a Yos 13:15, 17

b Hes 33:49

c Kum 23:27
Kum 34:1

d Hes 23:28

e Kum 2:26-28

f Hes 20:14, 17

Safu ya 2

a Kum 2:30-35
Kum 29:7
Amu 11:19, 20

b Zb 135:10, 11

c Hes 32:33
Ne 9:22d Hes 21:13
Kum 3:16

e Amu 11:21, 22

f Hes 32:1
1Nya 6:77, 81

g Yos 12:1, 2

h Mwa 10:15, 16
Mwa 15:16
Kut 3:8
Kum 7:1i Amu 11:23, 24
1Fa 11:7
2Fa 23:13

j Yos 13:15, 17

k Yos 13:8, 9

wapitie katika eneo lake. Badala yake, Sihoni akawakusanya watu wake wote kwenda kuwashambulia Waisraeli nyikani, akafika Yahazi na kuanza kupigana nao.^a **24** Lakini Waisraeli wakamshinda kwa upanga^b na kumiliki nchi yake^c kuanzia Arnoni^d mpaka Yaboki,^e karibu na Waamoni, kwa sababu jiji la Yazeri^f lina-pakana na eneo la Waamoni.^g

25 Basi Waisraeli wakachukua majiji hayo yote, wakaa-nza kuishi katika majiji yote ya Waamori,^h huko Heshboni na miji yake yote. **26** Kwa maana Heshboni lilikuwa jiji la Sihoni, mfalme wa Waamori ambaye alikuwa amepigana na mfalme wa Moabu na kuchukua nchi yake yote mpaka Arnoni. **27** Ndiyo maana watu walitunga shairi hili la dhihaka:

"Njooi Heshboni.

Jiji la Sihoni na lijengwe
na kuimarishwa kabisa.

28 Kwa maana moto ulitoka Heshboni, mwali wa moto ulitoka katika mji wa Sihoni.

Umeteketeza jiji la Ari
la Moabu, mabwana wa milima ya Arnoni.

29 Ole wako, Moabu! Mtaangamizwa, enyi watu wa Kemoshi!ⁱ

Huwafanya wanawe kuwa wakimbizi na binti zake kuwa mateka wa Sihoni, mfalme wa Waamori.

30 Acheni tuwapige mishale; Heshboni litaangamizwa mpaka Diboni;^j Acheni tuliharibu kabisa mpaka Nofa; Moto utasambaa mpaka Medeba."^k

31 Basi Waisraeli wakaanza kuishi katika nchi ya Waamori. **32** Kisha Musa akawatu ma watu fulani wakapeleleze Yazeri.^a Wakateka miji yake na kuwafukuza Waamori walio kuwa humo. **33** Halafu wakageuka na kupanda kupitia Njia ya Bashani. Ndipo Ogu^b mfalme wa Bashani akatoka pamoja na watu wake wote ili kupigana vita nao huko Edrei.^c **34** Yehova akamwambia Musa: “Usimwogope,^d kwa maana nitamtia mikononi mwako pamoja na watu wake wote na nchi yake,^e nawe utamteenda kama ulivyomteenda Sihoni mfalme wa Waamori, aliyeishi Heshboni.”^f **35** Basi wakaendelea kumshambulia pamoja na wanawe na watu wake wote hivi kwamba hakuna mtu yeyote kati ya watu wake aliyekoka,^g nao wakachukua nchi yake.^h

22 Kisha Waisraeli wakao ndoka na kupiga kambi kwenye jangwa tambarare la Moabu ng'ambo ya Yordani kutoka Yeriko.ⁱ **2** Sasa Balaki^j mwana wa Sipori aliona mambo yote ambayo Waisraeli waliwatendea Waamori, **3** na Wamoabu wakawaogopa sana Waisraeli, kwa sababu walikuwa wengi sana; naam, Wamoabu wakafadhaika kwa hofu kwa sababu ya Waisraeli.^k **4** Basi Wamoabu wakawaambia wazee wa Midiani: “Sasa umati huu utaramba eneo letu lote kama ng'ombe dume anavyokula nyasi shambani.”

Balaki mwana wa Sipori ndiye aliyekuwa mfalme wa Moabu wakati huo. **5** Aliwatumba wajumbe kwa Balaamu mwana wa Beori huko Petho-

SURA YA 21

a Hes 32:1

b Kum 3:11
Kum 4:47
Yos 13:8, 12c Kum 3:1
Kum 3:8, 10

d Kum 20:3

e Kut 23:27
Kum 7:24f Kum 3:2
Zb 135:10, 11

g Kum 3:3

h Yos 12:4-6

SURA YA 22

i Hes 33:48

j Yos 24:9
Amu 11:25k Kut 15:15
Kum 2:25l Hes 31:7, 8
Yos 13:15, 21

Safu ya 2

a Kum 23:3, 4
Yos 13:22
2Pe 2:15

b Mwa 13:14, 16

c Hes 23:7
Yos 24:9
Ne 13:1, 2d 2Pe 2:15
Yud 11

e Hes 22:20

f Hes 22:5, 6
Hes 23:7, 11
Hes 24:10g Mwa 12:1-3
Mwa 22:15, 17
Kum 33:29

ri,^a karibu na Mto Efrati katika nchi yake. Alimwambia hivi: “Sasa, kuna watu ambao wametoka Misri. Wamejaa kila mahali duniani,^{*b} na wana kaa papa hapa karibu nami. **6** Basi, tafadhali, njoo uwalaani watu hawa kwa niaba yangu,^c kwa maana wana nguvu kuliko mimi. Huenda nikawashinda na kuwafukuza kutoka nchini, kwa maana najua vema kwamba yule unayembariki amebarikiwa na yule unayemlaani amelaaniwa.”

7 Basi wazee wa Moabu na wazee wa Midiani wakachukua malipo ya uaguzi^{*} na kwenda kumwona Balaamu,^d wakamwambia maneno ya Balaki. **8** Ndipo Balaamu akawaambia: “Laleni hapa usiku wa leo, nami nitawajulisha jambo lolote ambalo Yehova ataniambia.” Hivyo wakuu wa Moabu wakakaa na Balaamu.

9 Kisha Mungu akamtokea Balaamu na kumuuliza:^e “Wanaume hawa walio pamoja nawe ni nani?” **10** Balaamu akamwambia Mungu wa kweli: “Balaki mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu, amenitumia ujumbe akisema, **11** ‘Watu wanaotoka Misri wamejaa kila mahali duniani. * Sasa njoo uwalaani kwa niaba yangu.’^f Huenda nikapigana nao na kuwafukuza.” **12** Lakini Mungu akamwambia Balaamu: “Usiende na wanaume hawa. Usiwalaani watu hao, kwa maana wamebarikiwa.”^g

13 Balaamu akaamka asubuhi na kuwambia wakuu wa Balaki: “Rudini katika nchi yenu, kwa maana Yehova amenikataza kwenda pamoja

22:5, 11 *Au “nchini.” 22:7 *Au “ubashiri.”

nanyi.” **14** Kwa hiyo wakuu wa Moabu wakaondoka, wakarudi kwa Balaki na kumwambia: “Balaamu amekataa kuja pamoja nasi.”

15 Hata hivyo, Balaki akawatama tena wakuu wengine, wengi zaidi na wengine kuheshimika zaidi kuliko wale wa kwanza. **16** Wakafika kwa Balaamu na kumwambia: “Balaki mwana wa Sipori anasema hivi: ‘Tafadhali, usiruhusu chochote kikuzuie kuja kwangu, **17** kwa maana nitakuthawabisha sana, nami nitafanya chochote utakachoniambia. Njoo tafadhali, uwalaani watu hawa kwa niaba yangu.’” **18** Lakini Balaamu akawaambia watumishi wa Balaki: “Hata Balaki akini nipa nyumba yake mwenyewe iliyojaa fedha na dhahabu, siwezi kukiuka jambo lolote ambalo Yehova Mungu wangu ameniagiza nifanye, liwe jambo dogo au kubwa.”^a **19** Lakini tafadhalini, laleni hapa usiku wa leo pia, ili nijue Yehova ataniambia jambo gani lingine.”^b

20 Kisha Mungu akamtoka Balaamu usiku na kumwambia: “Ikiwa wanaume hao wamekuja kukuita, nenda pamoja nao. Lakini utasema tu maneno nitakayokwambia.”^c **21** Basi Balaamu akaamka asubuhi, akaweka matandiko juu ya punda wake na kwenda pamoja na wakuu wa Moabu.^d

22 Lakini Mungu akakasirika sana kwa sababu Balaamu alikuwa akienda, na malaika wa Yehova akasimama njiani ili kumzuia. Sasa Balaamu alikuwa amepanda juu ya punda wake, na watumishi wake wawili walikuwa pamo-

SURA YA 22

a Hes 24:13

b Hes 22:8

c Hes 22:35
Hes 23:11, 12d 2Pe 2:15
Yud 11

Safu ya 2

a 2Pe 2:15, 16

b Hes 22:32

ja naye. **23** Punda huyo alipomwona malaika wa Yehova amesimama njiani akiwa ameshika upanga uliochomolewa, alijaribu kutoka njiani ili aingie shambani. Lakini Balaamu akaanza kumpiga punda huyo ili arudi njiani. **24** Ndipo malaika wa Yehova akasimama kwenye kijia chembamba katikati ya mashaamba mawili ya mizabibu, na kulikuwa na ukuta wa mawe upande huu na huu wa kijia hicho. **25** Punda alipomwona malaika wa Yehova, akaanza kujisukumiza ukutani na kuubana mguu wa Balaamu ukutani, na Balaamu akaanza kumpiga tena.

26 Sasa malaika wa Yehova akaenda mbele tena na kusimama mahali pembamba ambapo hapakuwa na nafasi ya kugeuka kulia au kushoto. **27** Punda alipomwona malaika wa Yehova, akalala chini Balaamu akiwa mgononi, basi Balaamu akakasirika sana na kuendelea kumpiga punda kwa fimbo yake. **28** Mwishowe Yehova akamfanya punda huyo aongee,^{*a} akamuuliza Balaamu: “Nimekutendea nini hivi kwa mba umenipiga mara tatu?”^b **29** Balaamu akamjibu hivi punda huyo: “Ni kwa sababu umenifanya mjinga. Ningekuwa na upanga mkononi, ningekuua!” **30** Kisha punda akamwambia Balaamu: “Je, mimi si punda wako ambaye amekubeba maisha yako yote mpaka leo? Je, nimewahi kukutendea hivi?” Balaamu akajibu: “Hapana!” **31** Ndipo Yehova akayafungua macho ya

22:28 *Tnn., “akakifungua kinywa cha huyo punda jike.”

Balaamu,^a naye akamwona malaika wa Yehova amesi-mama njiani akiwa ameshika upanga uliochomolewa. Papo hapo Balaamu akainama chini na kusujudu.

32 Malaika wa Yehova akamwambia: “Kwa nini umempiga punda wako mara tatu? Mimi mwenyewe nimekuja kukuzua kwa sababu njia yako haipatani na mapenzi yangu.^b **33** Punda aliniona na kujaribu kunikwepa mara hizo tatu.^c Kama hangenikwepa ningekuwa nimekuua na kumwacha yeye akiwa hai.”

34 Balaamu akamwambia malaika wa Yehova: “Nimeta-nda dhambi, kwa sababu sikujua kwamba ni wewe uliyesimama njiani ili kunizuia. Na sasa ikiwa hufurahii jambo hili, mimi nitarudi.” **35** Lakini malaika wa Yehova akamwambia Balaamu: “Nenda pamoja na wanaume hao, lakini utasema tu maneno nitakayokwambia.” Basi Balaamu akaendelea na safari pamoja na wakuu wa Balaki.

36 Balaki aliposikia kwamba Balaamu amefika, alitoka nje mara moja kumpokea katika jiji la Moabu, kwenye ukingo wa Arnoni, katika mpaka wa Moabu. **37** Balaki akamuuliza Balaamu: “Je, sikuwatuma wajumbe wakuite uje kwangu? Kwa nini hukuja? Je, ulidhani siwezi kukuthawabisha kwelikweli?”^d **38** Balaamu akamjibu hivi Balaki: “Sasa nimekuja kwako. Lakini, je, nitaruhusiwa kusema jambo lolote? Ninaweza kusema tu maneno ambayo Mungu anatia kinywani mwangu.”^e

39 Kwa hiyo Balaamu akaenda pamoja na Balaki, wakafi-

SURA YA 22

a 2Fa 6:17

b Hes 22:12
2Pe 2:15, 16c Hes 22:23
Hes 22:25
Hes 22:27d Hes 22:16, 17
Hes 24:10, 11e Hes 23:26
Hes 24:13

Safu ya 2

a Hes 23:13, 14

SURA YA 23

b Hes 22:41

c Hes 23:13, 14
Hes 23:28-30

d Hes 22:20

e Hes 22:35

f Hes 23:18
Hes 24:3g Mwa 10:22
Hes 22:5
Kum 23:3, 4

ka Kiriath-husothi. **40** Balaki akatoa dhabihu za ng'ombe na kondoo, naye akamgawia Balaamu na wakuu waliokuwa pamoja naye. **41** Asubuhi Balaki akamchukua Balaamu na kwenda naye Bamothbaali; akiwa huko aliweza kuwaona Waisraeli wote.^a

23 Kisha Balaamu akamwambia Balaki: “Jenga madhabahu saba mahali hapa,^b nawe unitayari-shie ng'ombe dume saba na kondoo dume saba.” **2** Mara moja Balaki akafanya kama Balaamu alivyomwambia. Kisha Balaki na Balaamu wakatoa dhabihu ya ng'ombe dume mmoja na kondoo dume mmoja juu ya kila madhabahu.^c

3 Halafu Balaamu akamwambia Balaki: “Kaa hapa karibu na dhabihu yako ya kuteketezwa, nami nitaenda. Labda Yehova atawasiliana nami. Jambo lolote atakalonifunulia, nitakwambia.” Basi akaenda juu ya kilima kilicho wazi.

4 Ndipo Mungu akawasiliana na Balaamu,^d Balaamu akamwambia: “Nilijenga safu za madhabahu saba na kutoa dhabihu ya ng'ombe dume mmoja na kondoo dume mmoja juu ya kila madhabahu.”

5 Yehova akatia maneno haya katika kinywa cha Balaamu:^e “Rudi kwa Balaki, na hili ndilo utakalosema.” **6** Basi akarudi na kumkuta Balaki na wakuu wote wa Moabu wakiwa wamesimama karibu na dhabihu yake ya kuteketezwa. **7** Kisha akasema maneno haya ya kishairi:^f

“Balaki mfalme wa Moabu amenileta kutoka Aramu,^g

Kutoka katika milima ya mashariki:

‘Njoo umlaani Yakobo kwa niaba yangu.

Naam, njoo uwashutumu Waisraeli.’^a

8 Ninawezaje kuwalaani watu ambao Mungu haja-walaani?

Ninawezaje kuwashutumu wale ambao Yehova haja-washutumu?^b

9 Kutoka juu ya miamba ninawaona,

Na kutoka vilimani ninawatazama.

Wanaishi peke yao kama taifa;^c

Hawajioni kuwa sawa na mataifa mengine.^d

10 Ni nani anayeweza kuhesabu chembe za mavumbi ya Yakobo^e

Au hata kuhesabu robo ya Waisraeli?

Acha nife kifo cha watu wanyoofu,

Na mwisho wangu uwe kama wao.”

11 Ndipo Balaki akamwambia Balaamu: “Kwa nini umenitendea hivi? Nilikuleta ili uwalaani maadui wangu, lakini badala yake umewabariki tu.”^f **12** Balaamu akasema: “Je, sipaswi kusema neno lote ambalo Yehova anatia kinywani mwangu?”^g

13 Balaki akamwambia: “Tafadhali, twende mahali pengine ambapo unaweza kuwaona. Utaona baadhi yao; hutawaona wote. Ukiwa huko walaani kwa niaba yangu.”^h

14 Kwa hiyo akampeleka kwenye uwanja wa Sofimu, juu ya Pisga,ⁱ naye akajenga madhabahu saba na kutoa dhabihu

SURA YA 23

a Hes 22:6

b Hes 22:12

c 1Fa 8:53

d Kut 33:16

e Mwa 13:14, 16
Mwa 22:17
Kut 1:7

f Hes 24:10
Yos 24:10
Ne 13:1, 2

g Hes 22:38
Hes 24:13

h Hes 22:11

i Kum 34:1

Safu ya 2

a Hes 22:41
Hes 23:1
Hes 23:28, 29

b Hes 22:35
Hes 23:5

c Hes 23:7
Hes 24:3

d Zb 89:35
Tit 1:2

e 1Sa 15:29

f Isa 14:24
Isa 46:10
Mik 7:20

g Mwa 12:1, 2
Mwa 22:15, 17
Hes 22:12

h Hes 22:18

i Kut 13:21
Kut 23:20
Kut 29:45
Isa 8:10

j Kut 20:2

k Hes 24:8

ya ng’ombe dume mmoja na kondoo dume mmoja juu ya kila madhabahu.^a **15** Kisha Balaamu akamwambia Balaki: “Kaa hapa karibu na dhabihu yako ya kuteketezwa ninapoe-nda pale kuwasiliana Naye.” **16** Basi Yehova akawasiliana na Balaamu na kutia neno hili kinywani mwake:^b “Rudi kwa Balaki, na hili ndilo utakalosema.” **17** Basi akarudi na kumkuta Balaki akisubiri karibu na dhabihu yake ya kuteketezwa, na wakuu wa Moabu walikuwa pamoja naye. Balaki akamuuliza: “Yehova amesema nini?” **18** Kisha Balaamu akasema maneno haya ya kishairi:^c

“Inuka, Balaki, usikilize. Nisikilize, ewe mwana wa Sipori.

19 Mungu si mwanadamu anayesema uwongo,^d

Wala si binadamu anayebadili nia yake.^{*e}

Akisema jambo, je, hatalitenda?

Akinena jambo, je, hatalitimiza?^f

20 Tazama! Nimeletwa ili ni-bariki;

Sasa Yeye amebariki,^g nami siwezi kubadili.^h

21 Havumilii nguvu zozote za uchawi dhidi ya Yakobo, Wala haruhusu taabu yoyote impate Israeli.

Yehova Mungu wake yuko pamoja nao,ⁱ

Nao humsifu kwa sauti kubwa kuwa mfalme wao.

22 Mungu anawatoa Misri.^j Yeye ni kama pembe za fahali mwitu.^k

23:19 *Au “anayejuta.”

23 Kwa maana hakuna ishara za msiba dhidi ya Yakobo,^a Wala hakuna uaguzi* wote dhidi ya Israeli.^b Sasa inaweza kusemwa hivi kuhusu Yakobo na Israeli:

“Tazameni mambo ambayo Mungu ametenda!”

24 Watu hawa watainuka kama simba, Na kama simba, watajiinua.^c Hawatalala chini mpaka wale mawindo Na kunywa damu ya waliouawa.”

25 Ndipo Balaki akamwambia Balaamu: “Ikiwa huwezi kamwe kuwalaani, basi usiwariki pia.” **26** Balaamu akamwambia Balaki: “Je, siku kwambia, ‘Nitafanya mambo yote ambayo Yehova anasema?’”^d

27 Ndipo Balaki akamwambia Balaamu: “Tafadhali njoo nikupeleke mahali pengine. Labda Mungu wa kweli atakubali uwalaani kwa niaba yangu kutoka mahali hapo.”^e

28 Basi Balaki akampeleka Balaamu juu ya Mlima Peori, unaoelekeana na Yeshimoni.^{*f}

29 Kisha Balaamu akamwambia Balaki: “Jenga madhabahu saba mahali hapa, nawe unitayarishie ng’ombe dume saba na kondoo dume saba.”^g

30 Kwa hiyo Balaki akafanya kama Balaamu alivyomwambia, naye akatoa dhahihu ya ng’ombe dume mmoja na kondoo dume mmoja juu ya kila madhabahu.

23:23 *Au “ubashiri.” 23:28 *Au labda, “jangwa; nyika.”

SURA YA 23

a Mwa 12:1, 3

b Hes 22:7

c Hes 24:9

d Hes 22:38
Hes 23:12

e Hes 23:13

f Hes 21:20

g Hes 22:41
Hes 23:1, 14

Safu ya 2

SURA YA 24

a Hes 23:3, 15
Hes 23:23b Hes 2:2
Hes 23:9

c 1Sa 19:20

d Hes 23:7, 18

e Hes 24:16

f Hes 1:52
Hes 2:2

g Hes 22:11

h Kum 8:7

i Mwa 49:10
Zb 2:6
Yoh 1:49

j Hes 24:20

k 1Nya 14:2
Da 2:44
Ufu 11:15

24 Balaamu alipoona kwa mba Yehova alifurahia* kuwabariki Waisraeli, hakwenda tena kutafuta ishara za msiba,^a bali aliugeuza uso wake kutazama nyikani. **2** Balaamu alipotazama na kuwaona Waisraeli wakiwa wamepiga kambi kulingana na makabila yao,^b roho ya Mungu ikamjia.^c **3** Kisha akasema maneno haya ya kishairi:^d

“Maneno ya Balaamu mwana wa Beori,
Na maneno ya mwanamu-me ambaye macho yake yamefunguliwa,

4 Maneno ya mtu anayesikia neno la Mungu,
Aliyeona maono ya Mweza-Yote,
Aliyeinama chini macho yakiwa yamefunguliwa:^e

5 Mahema yako yanapendeleza sana, Ee Yakobo,
Makao yako, Ee Israeli!^f

6 Yameenea mbali kama mabonde,^g
Kama bustani kando ya mto,
Kama mimea ya udi iliyo pandwa na Yehova,
Kama mierezi kando ya maji.

7 Maji yanaendelea kutiririka kutoka katika ndoo zake mbili za ngozi,
Na mbegu yake ime pandwa* kando ya maji mengi.^h

Mfalme wakeⁱ pia atakuwa mkuu kuliko Agagi,^j
Na ufalme wake utakwezwa.^k

24:1 *Tnn., “lilikuwa jambo jema machoni pa Yehova.” 24:7 *Au “uzao wake umepandwa.”

8 Mungu anamtoa Misri; Yeye ni kama pembe za fahali mwitu kwa Wais-raeli.

Atayala mataifa, wale wa-naomkandamiza,^a

Na mifupa yao ataitafuna-tafuna, naye atawapasua-pasua kwa mishale yake.

9 Amejikunyata, amelala chini kama simba,

Na kama simba, ni nani anayethubutu ku-mwamsha?

Wale wanaokubariki wamebarikiwa,

Na wale wanaokulaani wamelaaniwa.”^b

10 Ndipo Balaki akamkasi-rikia sana Balaamu. Akapiga makofi kwa dharau na ku-mwambia Balaamu: “Nilikuita uwalaani maadi wangu,^c badala yake umewabariki mara tatu. **11** Sasa rudi nyumbani mara moja. Nilitaka kukutha-wabisha sana,^d lakini Yehova amekunyima thawabu.”

12 Balaamu akamwambia Balaki: “Je, sikuwaambia hivi wajumbe uliowatuma kwangu:

13 ‘Hata Balaki akinipa nyumba yake mwenyewe iliyojaa fedha na dhahabu, siwezi kwa hiari yangu* kukiuka jambo lolote ambalo Yehova ameni-giza nifanye, liwe jambo zuri au baya. Nitasema tu jambo ambalo Yehova ataniambia?’^e

14 Na sasa naenda kwa watu wangu. Njoo nikwambie* mambo ambayo watu hawa watawatendea watu wako wa-kati ujao.”^f **15** Kwa hiyo

24:13 *Tnn., “kutoka moyoni mwangu.”

24:14 *Au “nikupe ushauri kuhusu.”
*Au “siku za mwisho.”

SURA YA 24

a Kut 23:27
Kum 9:5

b Mwa 12:1-3
Mwa 27:29

c Hes 22:10, 11
Hes 23:11
Ne 13:1, 2

d Hes 22:16, 17

e Hes 22:18, 38

Safu ya 2

a Hes 23:7

b Hes 24:3, 4

c Ufu 22:16

d Zb 110:2
Ebr 1:8

e 2Sa 7:16, 17
Isa 9:7

f 2Sa 8:2
1Nya 18:2
Zb 108:9

g Mwa 27:37
2Sa 8:14
Amo 9:11, 12

h Mwa 36:8
Yos 24:4

i 1Nya 4:42, 43
Eze 25:14

j Mwa 49:10
Zb 2:9
Zb 72:11
Ufu 6:2
Ufu 19:15

k Kut 17:8, 14

l Kum 25:19
1Sa 15:3
1Nya 4:43

m Mwa 15:18, 19
Amu 1:16

akasema maneno haya ya kishairi:^a

“Maneno ya Balaamu mwana wa Beori,

Na maneno ya mwanamu-me ambaye macho yake yamefunguliwa,^b

16 Maneno ya mtu anayesikia neno la Mungu,

Na yule anayemjua Aliye Juu Zaidi,

Aliona maono ya Mweza-Yote

Alipokuwa akiinama chini macho yake yakiwa yamefunguliwa:

17 Nitamwona, lakini si sasa; Nitamtazama, lakini si hivi karibuni.

Nyota^c itatoka kwa Yakobo,

Na fimbo ya ufalme^d itainuka katika Israeli.^e

Naye hakika atapasua paji la uso la Moabu^f

Na fuvu la kichwa la wana wote wa vurugu.

18 Na Edomu itamilikiwa,^g

Naam, Seiri^h itamilikiwa na maadi wake,ⁱ

Huku Israeli ikidhihirisha ujasiri wake.

19 Na mzao wa Yakobo atakuwa akishinda,^j

Naye atamwangamiza yeyote atakayeokoka jijini.”

20 Alipowaona Waamaleki, aliendelea kusema maneno yake ya kishairi:

“Amaleki lilikuwa taifa la kwanza,^k

Lakini mwishowe litaangamia.”^l

21 Alipowaona Wakeni,^m aliendelea kusema maneno yake ya kishairi:

“Makao yenu yako salama, yamejengwa juu ya mwamba.

22 Lakini mtu fulani atawateketeza Wakeni.*

Ni muda gani unaobaki kabla ya Ashuru kuwachukua mateka?”

23 Akaendelea kusema maneno yake ya kishairi:

“Lo! Ni nani atakayeokoka Mungu atakapofanya hivyo?”

24 Meli zitatoka pwani ya Kitimu,^a

Zitashambulia Ashuru,^b Na kushambulia Eberi.

Lakini wao pia wataangamia* kabisa.”

25 Kisha Balaamu^c akaondoka na kurudi kwake. Balaam pia akaenda zake.

25 Waisraeli walipokuwa wakikaa Shitimu,^d watu walianza kufanya uasherati na mabinti wa Moabu.^e **2** Wana-wake hao waliwaalika kwenye dhabihu za miungu yao,^f nao watu wakaanza kula na kuinama miungu yao.^g **3** Kwa hiyo Waisraeli wakashiriki katika kumwabudu* Baali wa Peori,^h na hasira ya Yehova ikawaka dhidi yao. **4** Yehova akamwambia Musa: “Wachukue viongozi wote wa watu hawa na uwatundike kweupe kabisa wakati wa mchana* mbele za Yehova, ili hasira kali ya Yehova isiendeleo kuwaka dhidi ya Waisraeli.” **5** Kisha Musa akawaambia hivi waamuzi wa Israeli:ⁱ “Kila mmoja wenu awaue watu wake wa-

24:22 *Tnn., “ataliteketeza Kaini.”

24:24 *Tnn., “yeye pia ataangamia.”

25:3 *Au “wakashikamana na.” 25:4 *Au “juani.”

SURA YA 24

a Mwa 10:2, 4
Eze 27:6

b Nah 3:18

c Hes 31:7, 8

SURA YA 25

d Yos 2:1
Mik 6:5

e Hes 31:16
IKo 10:8
Ufu 2:14

f Kut 34:15
IKo 10:20

g Kut 20:5

h Kum 4:3
Yos 22:17
Zb 106:28, 29
Ho 9:10

i Kut 18:21

Safu ya 2

a Kut 22:20
Kut 32:25, 27
Kum 13:6-9

b Hes 25:14, 15

c Kut 6:25
Yos 22:30

d Zb 106:30

e Hes 25:4
Kum 4:3
IKo 10:8

f Hes 25:7

g Zb 106:30, 31

h Kut 20:5
Kut 34:14
Kum 4:24

i INya 6:4
Ezr 7:1, 5
Ezr 8:1, 2

j IFa 19:10

lioshiriki katika kumwabudu* Baali wa Peori.”^a

6 Lakini wakati huo, Mwisraeli fulani akamleta mwanamke Mmidiani^b karibu na ndugu zake Waisraeli huku Musa na Waisraeli wote wakitazama walipokuwa wakilia kwenye mlango wa hema la mkutano.

7 Finehasi^c mwana wa Eleazari mwana wa kuhani Haruni alipoona jambo hilo, alinuka mara moja kutoka kati ya Waisraeli waliokusanyika, akachukua mkuki. **8** Kisha akamfuata mwanamume huyo Mwisraeli mpaka hemani, akawachoma mkuki wote wawili, nao ukapenya kwenye viungo vya uzazi vya mwanamke huyo. Ndipo pigo lililowapata Waisraeli likakomeshwa.^d **9** Watu waliokufa kutokana na pigo hilo walikuwa 24,000.^e

10 Kisha Yehova akamwambia Musa: **11** “Finehasi^f mwana wa Eleazari mwana wa kuhani Haruni amezuia ghadhabu yangu dhidi ya Waisraeli kwa sababu hakuvumilia ushindani wowote dhidi yangu miongoni mwao.^g Kwa hiyo sijawaangamiza Waisraeli licha ya kwamba ninasisitiza watu waniabudu mimi peke yangu.^h **12** Kwa hiyo mwambie, ‘Ninafanya agano langu la amani pamoja naye. **13** Nalo litakuwa agano la ukuhani wa kudumu kwa ajili yake na wazao wake,ⁱ kwa maana hakuvumilia ushindani wowote kumwelekea Mungu wake,^j naye alifanya dhambi ya Waisraeli ifunikwe.”

14 Sasa, mwanamume huyo Mwisraeli aliyeuawa pamoja na mwanamke Mmidiani alii-twa Zimri mwana wa Salu,

25:5 *Au “walioshikamana na.”

mkuu wa ukoo* wa Wasimeoni. **15** Mwanamke Mmidiani aliyeuawa aliiwa Kozbi binti ya Suri;^a Suri alikuwa kiongozi wa koo* za nyumba fulani huko Midiani.^b

16 Baadaye Yehova akamwambia Musa: **17** “Wachokozeni Wamidiani na kuwanamiza,^c **18** kwa sababu wamekuwa wakiwachokoa kwa hila zao kama ilivyokuwa kule Peori^d na pia kuhusiana na Kozbi binti ya mkuu wa Midiani, dada yao aliyeuawa^e wakati pigo lilipotokea kwa sababu ya mambo yaliyotokea Peori.”^f

26 Baada ya pigo hilo,^g Yehova akamwambia hivi Musa na Elezari mwana wa kuhani Haruni: **2** “Wahesabuni Waisraeli wote wenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi, kulingana na koo zao,* wahesabuni wote wanaoweza kutumikia katika jeshi la Israeli.”^h **3** Basi Musa na kuhani Elezariⁱ wakaambua watu hivi katika jangwa tambarare la Moabu/ karibu na Yordani huko Yeriko:^k **4** “Wahesabuni watu wenye umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi, kama Yehova alivyomwamuru Musa.”^l

Kwa hiyo Waisraeli waliotoka nchini Misri walikuwa: **5** Rubeni,^m mzaliwa wa kwanza wa Israeli; wana wa Rubeniⁿ walikuwa: kutoka kwa Hanoki, ukoo wa Wahanoki; kutoka kwa Palu, ukoo wa Wapalu; **6** kutoka kwa Hezroni, ukoo wa Wahezroni; kutoka kwa Karmi, ukoo wa Wakarmi. **7** Hizo ndizo zilizokuwa koo za Warubeni, na watu walioa-

25:14, 15; 26:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 25

a Hes 31:7, 8
Yos 13:21

b INya 1:32, 33

c Hes 31:1, 2

d Hes 25:3
Hes 31:16

e Hes 25:8, 15

f Hes 25:9

SURA YA 26

g Hes 25:7, 8

h Kut 30:12
Kut 38:26
Hes 1:2

i Hes 20:26

j Hes 22:1
Hes 33:48

k Yos 6:1

l Hes 1:3

m Mwa 29:32

n Mwa 46:8, 9
Kut 6:14

Safu ya 2

a Hes 1:21

b Hes 16:12

c Hes 16:1

d Hes 16:5, 19
Kum 11:6
Zb 106:17

e Hes 16:32, 35
Zb 106:18

f Hes 16:38
IKo 10:10, 11

g Kut 6:24
Hes 26:58
Zb 42:Uta

h Mwa 35:23
Mwa 46:10
Kut 6:15
INya 4:24

i Hes 1:23

j Mwa 35:26
Mwa 46:16

k Hes 1:25

l Mwa 29:35
Mwa 46:12

m Mwa 38:2-4

n Mwa 38:7-10

ndikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 43,730.^a

8 Mwana wa Palu alikuwa Eliabu. **9** Na wana wa Eliabu walikuwa Nemueli, Dathani, na Abiramu. Huyu ndiye Dathani na Abiramu, wakuu wa Waisraeli ambao walimpinga Musa^b na Haruni na kujiunga na kikundi cha Kora:^c kili-chompinga Yehova.^d

10 Kisha dunia ikafunguka* na kuwameza. Lakini Kora alikufa pamoja na watu walio muunga mkono moto ulipowateketeza watu 250.^e Wakawa onyo kwa wengine.^f **11** Hata hivyo, wana wa Kora hawakufa.^g

12 Wana wa Simeoni^h kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa Nemueli, ukoo wa Wanemueli; kutoka kwa Yamini, ukoo wa Wayamini; kutoka kwa Yakini, ukoo wa Wayakini; **13** kutoka kwa Zera, ukoo wa Wazera; kutoka kwa Shauli, ukoo wa Washauli. **14** Hizo ndizo zilizokuwa koo za Wasimeoni: walikuwa 22,200.ⁱ

15 Wana wa Gadi^j kulingana na koo zao: kutoka kwa Sefoni, ukoo wa Wasefoni; kutoka kwa Hagi, ukoo wa Wahagi; kutoka kwa Shuni, ukoo wa Washuni; **16** kutoka kwa Ozni, ukoo wa Waozni; kutoka kwa Eri, ukoo wa Waeri; **17** kutoka kwa Arodi, ukoo wa Waarodi; kutoka kwa Areli, ukoo wa Waareli. **18** Hizo ndizo zilizokuwa koo za wana wa Gadi, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 40,500.^k

19 Wana wa Yuda^l walikuwa Eri na Onani.^m Hata hivyo, Eri na Onani walikufa katika nchi ya Kanaani.ⁿ **20** Na wana wa

26:10 *Tnn., “ikafungua kinywa chake.”

Yuda kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa She-la,^a ukoo wa Washela; kutoka kwa Perezi,^b ukoo wa Wape-rezi; kutoka kwa Zera,^c ukoo wa Wazera. **21** Na wana wa Perezi walikuwa: kutoka kwa Hezroni,^d ukoo wa Wahezroni; kutoka kwa Hamuli,^e ukoo wa Wahamuli. **22** Hizo ndizo zilizokuwa koo za Yuda, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 76,500.^f

23 Wana wa Isakari^g kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa Tola,^h ukoo wa Watola; kutoka kwa Puva, ukoo wa Wapuni; **24** kutoka kwa Yashubu, ukoo wa Wayashubu; kutoka kwa Shimroni, ukoo wa Washimroni. **25** Hizo ndizo zilizokuwa koo za Isakari, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 64,300.ⁱ

26 Wana wa Zabuloni^j kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa Seredi, ukoo wa Waseredi; kutoka kwa Eloni, ukoo wa Waeloni; kutoka kwa Yahleeli, ukoo wa Wayahleeli. **27** Hizo ndizo zilizokuwa koo za Wazabuloni, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 60,500.^k

28 Wana wa Yosefu^l kulingana na koo zao walikuwa Manase na Efraimu.^m

29 Wana wa Manaseⁿ walikuwa: kutoka kwa Makiri,^o ukoo wa Wamakiri; naye Makiri alikuwa baba ya Gileadi;^p kutoka kwa Gileadi, ukoo wa Wagileadi. **30** Hawa ndio walio-kuwa wana wa Gileadi: kutoka kwa Yezeri, ukoo wa Wayeze-ri; kutoka kwa Heleki, ukoo wa Waheleki; **31** kutoka kwa Asrieli, ukoo wa Waasrieli; kutoka kwa Shekemu, ukoo wa

SURA YA 26

a Mwa 38:2, 5
Mwa 38:26
1Nya 4:21

b Mwa 38:29
Ru 4:18
Mt 1:3

c Mwa 38:30
1Nya 2:4

d Ru 4:19

e 1Nya 2:5

f Hes 1:27

g Mwa 30:18
Mwa 35:23
Mwa 46:13
1Nya 7:1

h 1Nya 7:2

i Hes 1:29

j Mwa 30:20
Mwa 46:14

k Hes 1:31

l Mwa 30:24
Mwa 35:24
Mwa 46:20

m Mwa 41:52

n Mwa 41:51

o Mwa 50:23
Kum 3:15
1Nya 7:14

p Yos 17:1

Safu ya 2

a Hes 27:7
1Nya 7:15

b Hes 36:11

c Hes 1:35

d Mwa 41:52

e 1Nya 7:20

f Hes 1:33
Yos 17:17

g Mwa 35:24
Mwa 46:21
1Nya 8:1

h 1Nya 7:6

i 1Nya 8:3, 4

j Hes 1:37

k Mwa 30:6

Washekemu; **32** kutoka kwa Shemida, ukoo wa Washemida; kutoka kwa Heferi, ukoo wa Waheferi. **33** Sasa Selofehadi mwana wa Heferi hakuwa na watoto wa kiume, alikuwa na mabinti tu,^a na majina ya mabinti wa Selofehadi^b ni Mala, Noa, Hogla, Milka, na Tirsia. **34** Hizo ndizo zilizo-kuwa koo za Manase, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 52,700.^c

35 Hawa ndio waliokuwa wana wa Efraimu^d kulingana na koo zao: kutoka kwa Shuthela,^e ukoo wa Washuthela; kutoka kwa Bekeri, ukoo wa Wabekeri; kutoka kwa Tahani, ukoo wa Watahani. **36** Na hawa ndio wana wa Shuthela: kutoka kwa Erani, ukoo wa Waerani. **37** Hizo ndizo zilizokuwa koo za wana wa Efraimu, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 32,500.^f Hao ndio waliokuwa wana wa Yosefu kulingana na koo zao.

38 Wana wa Benjamini^g kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa Bela,^h ukoo wa Wabela; kutoka kwa Ashbéli, ukoo wa Waashbéli; kutoka kwa Ahiramu, ukoo wa Waa-hiramu; **39** kutoka kwa Shefufamu, ukoo wa Washufamu; kutoka kwa Hufamu, ukoo wa Wahufamu. **40** Wana wa Bela ni Ardi na Naamani:ⁱ kutoka kwa Ardi, ukoo wa Waardi; kutoka kwa Naamani, ukoo wa Wanaamani. **41** Hao ndio waliokuwa wana wa Benjamini kulingana na koo zao, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 45,600.^j

42 Hawa ndio waliokuwa wana wa Dani^k kulingana

na koo zao: kutoka kwa Shuhamu, ukoo wa Washuhamu. Hizo ndizo zilizokuwa koo za Dani kulingana na wazao wao. **43** Watu walioandikishwa kutoka katika koo zote za Washuhamu walikuwa 64,400.^a

44 Wana wa Asheri^b kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa Imna, ukoo wa Waimna; kutoka kwa Ishvi, ukoo wa Waishvi; kutoka kwa Beria, ukoo wa Waberia; **45** kutoka kwa wana wa Beria: kutoka kwa Heberi, ukoo wa Waheberi; kutoka kwa Malkieli, ukoo wa Wamalkieli. **46** Binti ya Asheri alitwa Sera. **47** Hizo ndizo zilizokuwa koo za wana wa Asheri, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 53,400.^c

48 Wana wa Naftali^d kulingana na koo zao walikuwa: kutoka kwa Yahzeeli, ukoo wa Wayahzeeli; kutoka kwa Guni, ukoo wa Waguni; **49** kutoka kwa Yezeri, ukoo wa Wayezeri; kutoka kwa Shilemu, ukoo wa Washilemu. **50** Hizo ndizo zilizokuwa koo za Naftali kulingana na wazao wao, na watu walioandikishwa kutoka katika koo hizo walikuwa 45,400.^e

51 Wanaume wote Waisraeli walioandikishwa walikuwa 601,730.^f

52 Kisha Yehova akamwambia Musa hivi: **53** "Watu hao wanapaswa kugawiwa urithi wa nchi kulingana na orodha ya majina."^g **54** Unapaswa kuyapa makundi makubwa urithi mkubwa, na makundi madogo urithi mdogo.^h Kila kundi linapaswa kupewa

26:53 *Au "kulingana na idadi ya majina yaliyoorodheshwa."

SURA YA 26

a Hes 1:39

b Mwa 30:13
Mwa 35:26
Mwa 46:17
1Nya 7:30

c Hes 1:41

d Mwa 30:8
Mwa 35:25
Mwa 46:24
1Nya 7:13

e Hes 1:43

f Kut 38:26
Hes 1:46, 49
Hes 14:29

g Yos 11:23
Yos 14:1

h Hes 33:54

Safu ya 2

a Hes 34:13
Yos 14:2
Yos 17:4
Yos 18:6
Met 16:33

b Mwa 46:11
Kut 6:16

c Hes 3:19

d Kut 6:17
Hes 3:18

e Hes 3:27

f Kut 6:19
Hes 3:33

g Hes 3:20
1Nya 23:23

h Kut 6:24

i Kut 6:18
Hes 3:19

j Kut 2:1
Kut 6:20

k Kut 15:20
Mik 6:4

l Kut 6:23
Kut 24:9

m Law 10:1, 2
Hes 3:2, 4
1Nya 24:2

n Hes 3:39

o Hes 1:49

p Hes 18:24
Kum 10:9
Kum 14:27
Yos 14:3

urithi wake kulingana na idadi ya watu walioorodheshwa. **55** Hata hivyo, nchi inapaswa kugawanywa kwa kura.^a Watu wanapaswa kupokea urithi wao kulingana na majina ya makabila ya baba zao. **56** Kila urithi utagawanywa kwa kura, na makundi makubwa na madogo yatapewa urithi wao."

57 Sasa hawa ndio Walawi walioandikishwa^b kulingana na koo zao: kutoka kwa Gershoni, ukoo wa Wagershoni; kutoka kwa Kohathi,^c ukoo wa Wakohathi; kutoka kwa Merari, ukoo wa Wamerari. **58** Hizi ndizo zilizokuwa koo za Walawi: ukoo wa Walibni,^d ukoo wa Wahebroni,^e ukoo wa Wamali,^f ukoo wa Wamushi,^g ukoo wa Wakora.^h

Kohathi alikuwa baba ya Amramu.ⁱ **59** Na mke wa Amramu alikuwa Yokebedi,^j binti ya Lawi; Yokebedi alizaliwa nchini Misri. Naye alimzalia Amramu, Haruni na Musa na Miriamu dada yao.^k **60** Kisha Haruni akamzaa Nadabu, Abihu, Eleazari, na Ithamari.^l **61** Lakini Nadabu na Abihu walikufa kwa sababu ya kumtolea Yehova moto haramu.^m

62 Wanaume wote wenye umri wa kuanzia mwezi mmoja na zaidi walioandikishwa walikuwa 23,000.ⁿ Hawakuaandikishwa pamoja na Waisraeli wengine,^o kwa sababu hawakupaswa kupewa urithi miongoni mwa Waisraeli.^p

63 Hao ndio walioandikishwa na Musa na kuhani Eleazari walipowaandikisha Waisraeli katika jangwa tambarare la Moabu karibu na Yordani huko Yeriko. **64** Lakini hakuna hata mmoja wao aliyea-

ndikishwa na Musa na kuhani Haruni wakati walipowahe-sabu Waisraeli katika nyika ya Sinai.^a **65** Kwa maana Yehova alikuwa amesema hivi kuwahu: “Ni lazima wafe nyikani.”^b Kwa hiyo hakuna mwanamume hata mmoja kati yao aliyebaki isipokuwa Kalebua mwana wa Yefune na Yoshua mwana wa Nuni.^c

27 Kisha mabinti wa Selo-fehadi,^d mwana wa Heferi, mwana wa Gileadi, mwana wa Makiri, mwana wa Manase, wa koo za Manase mwana wa Yosefu, wakaja. Mabinti hao waliitwa Mala, Noa, Hogla, Milka, na Tirsu. **2** Wakasimama mbele ya Musa, kuhani Eleazari, mbele ya wakuu,^e na mbele ya Waisraeli wote kwenye mlango wa hema la mkutano, wakasema: **3** “Baba yetu alikufa nyikani, lakini hakuwa miongoni mwa kikundi kilichojiunga na Kora kumpinga Yehova,^f bali alikufa kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe naye hakuwa na mtoto yeyote wa kiume. **4** Kwa nini jina la baba yetu lipotee kutoka katika ukoo wake kwa sababu hakuwa na mtoto wa kiume? Tupe urithi miongoni mwa ndugu za baba yetu.” **5** Kwa hiyo Musa akawasilisha kesi yao mbele za Yehova.^g

6 Basi Yehova akamwambia Musa hivi: **7** “Mabinti wa Selofehadi wanasema ukweli. Kwa vyovyote vile unapaswa kuwapa urithi miongoni mwa ndugu za baba yao na urithi wa baba yao.^h **8** Nawe uwambie Waisraeli hivi: ‘Mtu aki-fa bila kuacha mtoto wa kiume, mtampa binti yake urithi wake. **9** Na ikiwa hana binti, mtawapa ndugu zake urithi

SURA YA 26

a Hes 1:2
Kum 2:14
1Ko 10:5

b Ebr 3:17

c Hes 14:29, 30
Yos 14:14
Yos 19:49

SURA YA 27

d Hes 26:33

e Kut 18:25, 26

f Hes 14:35
Hes 16:1, 2
Hes 16:19, 35

g Kut 18:15, 16
Kut 33:11
Law 24:11, 12

h Hes 36:2
Yos 17:3, 4

Safu ya 2

a Hes 33:47
Kum 32:48, 49

b Mwa 13:14, 15
Kum 3:27
Kum 32:52
Kum 34:1

c Hes 31:2
Kum 34:7

d Hes 20:24, 28
Hes 33:38
Kum 10:6
Kum 32:50

e Hes 20:10, 12
Kum 1:37

f Zb 106:32, 33

g Kum 1:2

h Yos 15:1

i Kum 34:9
Mdo 6:5, 6

j Kum 31:7

wake. **10** Na ikiwa hana ndugu, mtawapa ndugu za baba yake urithi wake. **11** Na ikiwa baba yake hana ndugu, mtampa urithi wake mtu wa karibu zaidi wa ukoo aliye na uhusiano wa damu naye. Uamuzi huu utakuwa sheria kwa Waisraeli, kama Yehova alivyomwamuru Musa.”

12 Kisha Yehova akamwambia Musa: “Panda mlima huu wa Abarimu,^a uione nchi nitakayowapa Waisraeli.^b **13** Baada ya kuiona, utakufa pia na kuzikwa pamoja na watu wako,^{*c} kama Haruni ndugu yako alivyozikwa,^d **14** kwa sababu Waisraeli walipokuwa wakigombana nami katika nyika ya Zini, mliasi agizo langu la kunitakasa mbele yao nilipowapa maji.^e Hayo ndiyo maji ya Meriba^f huko Kadeshi^g katika nyika ya Zini.”^h

15 Kisha Musa akamwambia hivi Yehova: **16** “Yehova, Mungu anayewapa watu wote uhai,^{*} naomba umchague mwanamume atakayewasimamia watu hawa **17** ili awatangulie na kuwaongoza katika mambo yote, ili watu hawa wa Yehova wasiwe kama kondoo wasio na mchungaji.” **18** Kwa hiyo Yehova akamwambia Musa: “Mchukue Yoshua mwana wa Nuni, mwana-mume aliye na roho,^{*} na uweke mikono yako juu yake.ⁱ **19** Kisha umsimamishe mbele ya kuhani Eleazari na mbele ya watu wote, nawe umweke kuwa kiongozi.^j **20** Utampa

27:13 *Tnn., “utakusanywa pia kwa watu wako.” Huu ni msemo wa kishairi unaorejelea kifo. **27:16** *Tnn., “Mungu wa roho za miili yote.” **27:18** *Au “mtazamo unaofaa.”

sehemu ya mamlaka* yako,^a ili Waisraeli wote wamsikilize.^b **21** Atasimama mbele ya kuhani Eleazari, ambaye atatumia Urimu^c kujua uamuzi wa Yehova kwa niaba yake. Kwa agizo lake, yeye na Waisraeli wote na watu wengine wote watatoka, na kwa agizo lake wataingia ndani.”

22 Kwa hiyo Musa akafanya kama Yehova alivyomwamuru. Akamchukua Yoshua na kumsimamisha mbele ya kuhani Eleazari na mbele ya watu wote, **23** akaweka mikono yake juu yake na kumweka kuwa kiongozi,^d kama Yehova alivyosema kupitia Musa.^e

28 Kisha Yehova akamwambia Musa, **2** “Wamuru hivi Waisraeli: ‘Hakikisheni kwamba mnanitolea toleo langu, chakula changu.* Ni lazima mnitolee kwa wakati uliowekwa dhabihu zangu zinazoteketezwa zenye harufu inayonipendeza.’^f

3 “Nawe uwaambie, ‘Hii ndiyo dhabihu inayochomwa kwa moto ambayo mtamtolea Yehova: mtatoa kwa ukawaida kila siku wanakondoo dume wawili wasio na kasoro wenye umri wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa.’^g **4** Mtamtoa mwanakondoo dume mmoja asubuhi, na mwanakondoo dume wa pili mtamtoa jioni kabla ya giza kuingia,^{*h} **5** pamoja na toleo la nafaka la sehemu ya kumi ya kipimo cha efa moja* ya unga laini ulio-

27:20 *Au “heshima.” 28:2 *Au “mkate wangu.” #Au “inayonituliza.” 28:4, 8 *Tnn., “katikati ya zile jioni mbili.” 28:5 *Sehemu ya kumi ya efa ilikuwa sawa na lita 2.2 au kilogramu 1.3 hivi. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 27

a Kum 1:38
Kum 31:3
Kum 34:10

b Yos 1:17

c Kut 28:30
1Sa 23:9
1Sa 28:6
Ne 7:65

d Hes 27:18

e Kum 3:28
Kum 31:14, 23

SURA YA 28

f 2Nya 8:13
Ne 10:32, 33

g Kut 29:38
Law 6:9
Eze 46:15

h Kut 29:39

Safu ya 2

a Kut 29:40
Hes 15:4

b Kut 29:38, 42
2Nya 2:4
Ezr 3:3

c Kut 29:39, 40

d Kut 29:41

e Kut 16:29
Kut 20:10
Eze 20:12

f Hes 28:3, 7

g Hes 10:10
1Nya 23:31
2Nya 2:4
Ne 10:32, 33

changanywa na robo ya hini* ya mafuta ya zeituni zilizopondwa.^a **6** Ni dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida,^b iliyoanzishwa kwenye Mlima Sinai, dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza[#] Yehova, **7** pamoja na toleo lake la kinywaji la robo ya hini kwa ajili ya kila mwanakondoo dume.^c Miminini kileo mahali patakatifu kikiwa toleo la kinywaji mbele za Yehova. **8** Nanyi mtamtoa mwanakondoo dume wa pili jioni kabla ya giza kuingia.* Mtamtoa pamoja na toleo la nafaka kama lile lililotolewa asubuhi pamoja na toleo lake la kinywaji. Mtamtoa akiwa dhabihu inayochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza[#] Yehova.^d

9 “Hata hivyo, siku ya Sabato,^e mnapaswa kutoa wanakondoo dume wawili wasio na kasoro wenye umri wa mwaka mmoja pamoja na toleo la nafaka la sehemu mbili za kumi za kipimo cha efa ya unga laini uliochanganywa na mafuta, pamoja na toleo lake la kinywaji. **10** Hiyo ndiyo dhabihu ya kuteketezwa ya Sabato, pamoja na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida pamoja na toleo lake la kinywaji.^f

11 “Mwanzoni mwa kila mwezi* mtamtolea Yehova dhabihu ya kuteketezwa ya ng’ombe dume wawili wachanga, kondoo dume mmoja, wanakondoo dume saba wasio na kasoro wote wa umri wa mwaka mmoja,^g **12** na to-

28:5 *Hini ilikuwa sawa na lita 3.67. Angalia Nyongeza B14. 28:6, 8 #Au “inayomtuliza.” 28:11 *Tnn., “miezi yenu.”

leo la nafaka la sehemu tatu za kumi za vipimo vya unga laini uliochanganywa na mafuta^a kwa ajili ya kila ng'ombe dume na toleo la nafaka la sehemu mbili za kumi za vipimo vya unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya kondoo dume mmoja,^b **13** na toleo la nafaka la sehemu moja ya kumi ya kipimo cha unga laini uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya kila mwanakondoo dume; mtavitoa vitu hivyo vi-kiwa dhabihu inayochochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza*^c Yehova. **14** Na matoleo ya kinywaji ya dhabihu hiyo yanapaswa kuwa nusu ya hini ya divai kwa ajili ya ng'ombe dume^d na sehemu ya tatu ya hini kwa ajili ya kondoo dume^e na robo ya hini kwa ajili ya mwanakondoo dume.^f Hiyo ndiyo dhabihu ya kuteketezwa inayopaswa kutolewa kila mwezi kwa mwaka mzima. **15** Pia, mwanambuzi mmoja anapaswa kutolewa kwa Yehova ili kuwa dhabihu ya dhambi; atolewa na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida pamoja na toleo lake la kinywaji.

16 "Siku ya 14 ya mwezi wa kwanza, itakuwa Pasaka ya Yehova.^g **17** Na siku ya 15 ya mwezi huo, kutakuwa na sherehe. Mikate isiyu na chachu italiwa kwa siku saba.^h **18** Katika siku ya kwanza kutakuwa na kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu. **19** Nanyi mta-ntolea Yehova dhabihu ya kuteketezwa inayochochomwa kwa moto ya ng'ombe dume wawili wachanga, kondoo dume

SURA YA 28

a Law 2:11

b Law 1:10

c Law 1:10, 13

d Hes 15:8, 10

e Hes 15:6, 7

f Hes 15:5

g Kut 12:14
Law 23:5
Kum 16:1
Eze 45:21
1Ko 5:7

h Kut 12:15
Law 23:6
1Ko 5:8

Safu ya 2

a Law 22:20, 22
Kum 15:21

b Law 2:1

c Kut 13:6

d Kut 12:16
Law 23:8
Kum 16:8

e Kut 23:16

f Law 23:15, 16

g Kut 34:22
Kum 16:10
Mdo 2:1

h Law 23:16, 21

i Law 23:16, 18

mmoja, na wanakondoo dume saba wote wa umri wa mwaka mmoja. Mnapaswa kutoa wanyama wasio na kasoro.^a

20 Mnapaswa kuwatoa pamoja na matoleo ya nafaka ya unga laini uliochanganywa na mafuta;^b sehemu tatu za kumi kwa ajili ya ng'ombe dume na sehemu mbili za kumi kwa ajili ya kondoo dume mmoja.

21 Mtatoa sehemu moja ya kumi kwa ajili ya kila mwanakondoo dume kati ya wale wanakondoo dume saba, **22** na pia mbuzi mmoja ili kuwa dhabihu ya dhambi kwa ajili ya kufunika dhambi zenu.

23 Mtatoa vitu hivyo pamoja na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa asubuhi kwa ukawaida. **24** Mtatoa vitu hivyo kama chakula[#] kwa njia ileile kila siku kwa siku saba, ni dhabihu inayochochomwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova. Inapaswa kutolewa na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida pamoja na toleo lake la kinywaji. **25** Siku ya saba mtakuwa na kusanyiko takatifu.^c Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu.^d

26 "Siku ya mavuno ya kwanza yaliyokomaa,^e mnapomtolea Yehova nafaka iliyotoka kuvunwa^f katika sherehe yenu ya majuma,^g mnapaswa kuwa na kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu.^h **27** Mtatoa ng'ombe dume wawili wachanga, kondoo dume mmoja, na wanakondoo dume saba wote wa umri wa mwaka mmoja kuwa dhabihu ya kuteketezwa yenye harufu inayompendeza* Yehova,ⁱ **28** pamoja na toleo

28:13, 24, 27 *Au "inayomtuliza."

28:24 [#]Tnn., "mkate."

la nafaka la unga laini uliochanganywa na mafuta; sehemu tatu za kumi kwa ajili ya kila ng'ombe dume, na sehemu mbili za kumi kwa ajili ya kondoo dume mmoja, **29** sehemu moja ya kumi kwa ajili ya kila mwanakondoo dume kati ya wale wanakondoo dume saba, **30** na pia mwanambuzi mmoja kwa ajili ya kufunika dhambi zenu.^a **31** Mtatoa vitu hivyo pamoja na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida pamoja na toleo lake la nafaka. Mtatoa wanyama wasio na kasoro,^b pamoja na matoleo yao ya kinywaji.

29 “Na siku ya kwanza ya mwezi wa saba, mtakuwa na kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu.^c Mnapaswa kupiga tarumbeta siku hiyo.^d **2** Mtatoa ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, wanakondoo dume saba wote wa umri wa mwaka mmoja kuwa dhabihu ya kuteketezwa yenye harufu inayompendeza* Yehova, wanyama wote hawapaswi kuwa na kasoro, **3** pamoja na toleo la nafaka la unga laini uliochanganywa na mafuta; sehemu tatu za kumi kwa ajili ya ng'ombe dume, sehemu mbili za kumi kwa ajili ya kondoo dume, **4** na sehemu ya kumi kwa ajili ya kila mwanakondoo dume kati ya wale wanakondoo dume saba, **5** na mwanambuzi dume mmoja ili kuwa dhabihu ya dhambi kwa ajili ya kufunika dhambi zenu. **6** Mtatoa vitu hivyo pamoja na dhabihu ya kuteketezwa ya kila mwe-

29:2, 6, 8 *Au “inayomtuliza.”

SURA YA 28

a Law 23:16, 19

b Law 1:3

SURA YA 29

c Law 23:24, 25

d Hes 10:2

Zb 81:3

Safu ya 2

a Hes 28:11-13

b Hes 28:3, 5

c Hes 28:6, 7

d Law 16:29

e Law 23:27-31

f Law 1:3
Law 22:22
Kum 15:21
Kum 17:1

g Law 16:3

zi na toleo lake la nafaka^a na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida pamoja na toleo lake la nafaka^b na matoleo yake ya kinywaji,^c mkifuata utaratibu wa kawaida wa kutoa dhabihu hizo, ili iwe dhabihu inayocho-mwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova.

7 “Na siku ya kumi ya mwezi huo wa saba mtakuwa na kusanyiko takatifu,^d nanyi mnapaswa kujitesa.* Hampaswi kufanya kazi yoyote.^e **8** Mtamtoa ng'ombe dume mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na wanakondoo dume saba wote wa umri wa mwaka mmoja kuwa dhabihu ya kuteketezwa yenye harufu inayompendeza* Yehova; wanyama wote hawapaswi kuwa na kasoro.^f **9** Mta-watoa pamoja na toleo lao la nafaka la unga laini uliochanganywa na mafuta; sehemu tatu za kumi kwa ajili ya ng'ombe dume, sehemu mbili za kumi kwa ajili ya kondoo dume mmoja, **10** sehemu ya kumi kwa ajili ya kila mwanakondoo dume kati ya wale wanakondoo dume saba, **11** na pia mbuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, mbali na dhabihu ya dhambi inayotolewa kwa ajili ya kufunika dhambi^g na dhabihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na matoleo yake ya kinywaji.

12 “Na siku ya 15 ya mwezi wa saba mtakuwa na kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu, nanyi mnapaswa kumfa-

29:7 *Kwa ujumla inaeleweka kwamba “kujitesa” kunamaanisha kujinyima kwa njia mbalimbali, kutia ndani kufunga.

nyia Yehova sherehe kwa siku saba.^a **13** Mtatoa ng'ombe dume wachanga 13, kondoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja kuwa dhabihu inayochomwa^b kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova; wanyama wote hawapaswi kuwa na kasoro.^c **14** Mtawatoa pamoja na toleo lao la nafaka la unga laini uliochanganywa na mafuta; sehemu tatu za kumi kwa ajili ya kila ng'ombe dume kati ya wale ng'ombe dume 13, sehemu mbili za kumi kwa ajili ya kila kondoo dume kati ya wale kondoo dume 2, **15** na sehemu ya kumi kwa ajili ya kila wanakondoo dume kati ya wale wanakondoo dume 14, **16** na pia mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, mbali na dhabihu ya kuteketewa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.^d

17 “Na siku ya pili mtatoa ng'ombe dume wachanga 12, kondoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja, wanyama wasio na kasoro,^e **18** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya hao ng'ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **19** na pia mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, mbali na dhabihu ya kuteketewa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na matoleo yake ya kinywaji.^f

20 “Na siku ya tatu mtatoa ng'ombe dume 11, ko-

SURA YA 29

a Kut 23:16
Law 23:34-36
Kum 16:13-15
Ne 8:14-18

b Ezz 3:4

c Law 22:22
Kum 17:1

d Hes 28:3-8

e Law 22:22
Kum 17:1

f Hes 28:3-8

Safu ya 2

a Law 22:22
Kum 17:1

b Hes 28:3-8

c Law 22:22
Kum 17:1

d Hes 28:3-8

e Kum 15:21
Kum 17:1

ndoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja, wanyama wasio na kasoro,^a **21** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya hao ng'ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **22** na pia mbuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, mbali na dhabihu ya kuteketewa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.^b

23 “Na siku ya nne mtatoa ng'ombe dume 10, kondoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja, wanyama wasio na kasoro,^c **24** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya hao ng'ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **25** na pia mwanambuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, mbali na dhabihu ya kuteketewa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.^d

26 “Na siku ya tano mtatoa ng'ombe dume 9, kondoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja, wanyama wasio na kasoro,^e **27** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya hao ng'ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **28** na pia mbuzi mmoja kwa ajili ya dhabihu ya dhambi, mbali na dhabihu ya kuteketewa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na

toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.^a

29 “Na siku ya sita mtatoo ng’ombe dume 8, kondoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja, wanyama wasio na kasoro,^b **30** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya hao ng’ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **31** na pia mbuzi mmoja kwa ajili ya dhambihu ya dhambi, mbali na dhambihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na matoleo yake ya kinywaji.^c

32 “Na siku ya saba mtaotoa ng’ombe dume 7, kondoo dume 2, na wanakondoo dume 14 wote wa umri wa mwaka mmoja, wanyama wasio na kasoro,^d **33** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya hao ng’ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **34** na pia mbuzi mmoja kwa ajili ya dhambihu ya dhambi, mbali na dhambihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.^e

35 “Siku ya nane mtaukuwa na kusanyiko takatifu. Hampaswi kufanya kazi yoyote ngumu.^f **36** Mtaotoa ng’ombe dume mmoja, kondoo dume mmoja, na wanakondoo dume saba wote wa umri wa mwaka mmoja kuwa dhambihu inayocho-mwa kwa moto yenye harufu inayompendeza* Yehova, wa-

SURA YA 29

a Hes 28:3-8

b Law 22:22
Kum 17:1

c Hes 28:3-8

d Law 22:22
Kum 17:1

e Hes 28:3-8

f Law 23:36, 39

Safu ya 2

a Law 22:22
Kum 17:1

b Hes 28:3-8

c Law 23:2
Kum 16:16

d Kum 12:5, 6

e Law 7:16
Law 22:21

f Law 1:3

g Law 2:1

h Hes 15:5

i Law 3:1

SURA YA 30

j Kut 18:25

k Mwa 28:20-22
Amu 11:30, 31

l Zb 132:1-5

m Kum 23:21
Zb 116:14
Zb 119:106
Mhu 5:4
Mt 5:33

n Zb 50:14
Zb 66:13

nyama wote hawapaswi kuwa na kasoro,^a **37** na toleo la nafaka na matoleo ya kinywaji kwa ajili ya huyo ng’ombe dume, kondoo dume, na wanakondoo dume kulingana na idadi yao, mkifuata utaratibu wa kawaida, **38** na pia mbuzi mmoja kwa ajili ya dhambihu ya dhambi, mbali na dhambihu ya kuteketezwa inayotolewa kwa ukawaida, pamoja na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.^b

39 “Mtamtolea Yehova dhambihu hizo wakati wa sherehe zenu za majira,^c mbali na dhambihu zenu za nadhiri^d na matoleo yenu ya hiari^e yakikwa dhambihu zenu za kuteketezwa;^f na pia matoleo yenu ya nafaka^g na matoleo yenu ya kinywaji^h na dhambihu zenu za ushirika.”ⁱ **40** Musa aliwambia Waisraeli mambo yote ambayo Yehova alimwamuru.

30 Kisha Musa akawambia hivi viongoziⁱ wa makabila ya Israeli: “Yehova ameamuru hivi: **2** Mwanamume akimwekea Yehova nadhiri^k au akiapa^l kuweka nadhiri ya kujinyima kitu fulani,* hapaswi kuvunja ahadi yake.^m Anapaswa kufanya kila jambo aliloapa kufanya.ⁿ

3 “Na binti anayeishi katika nyumba ya baba yake akimwekea Yehova nadhiri au akiweka nadhiri ya kujinyima kitu fulani **4** na baba yake akisikia nadhiri yake au nadhiri aliyo-weka ya kujinyima lakini asimpinge, basi ni lazima atimize nadhiri zake zote, kutia ndani kila nadhiri aliyoweka ya kujinyima kitu fulani. **5** Lakini baba yake akimkataza baada

29:36 *Au “inayomtuliza.”

30:2 *Au “akijifunga wajibu.”

ya kusikia kwamba binti yake ameweka nadhiri au nadhiri za kujinyima kitu fulani, basi hatatimiza nadhiri hizo. Yehova atamsamehe kwa sababu baba yake alimkataza.^a

6 "Hata hivyo, binti huyo akiolewa baada ya kuweka nadhiri au kuahidi kujinyima kitu fulani bila kufikiri **7** na mume wake akisikia nadhiri yake lakini asimpinge siku anayosikia kuhusu nadhiri hiyo, basi ni lazima binti huyo atimize nadhiri zake au nadhiri alizoweka za kujinyima kitu fulani. **8** Lakini mume wake akimkataza siku anayosikia kuhusu nadhiri hiyo, mume huyo anaweza kufuta nadhiri hiyo au ahadi ambayo mke wake aliweka bila kufikiri,^b na Yehova atamsamehe mke huyo.

9 "Lakini mjane au mwana-mke aliyetalikiwa akiweka nadhiri, atatimiza kila jambo ambalo aliahidi.

10 "Hata hivyo, ikiwa mwana-mke aliweka nadhiri au nadhiri ya kujinyima kitu fulani akiwa katika nyumba ya mume wake **11** na mume wake alisikia nadhiri yake lakini hakumpinga wala kumkataza, basi ni lazima atimize nadhiri zake au nadhiri yoyote aliyoweka ya kujinyima kitu fulani. **12** Lakini ikiwa mume wake alifuta kabisa nadhiri zozote au nadhiri yoyote ya kujinyima ya mke wake siku aliposikia kuzihusu, mke wake hatatimiza nadhiri hizo.^c Mume wake alizifuta, na Yehova atamsamehe mke huyo. **13** Mume wake anapaswa kukubali au kufuta kiapo chochote au nadhiri yoyote ya kujinyima kitu fulani. **14** Laki-

SURA YA 30

a Kut 20:12

b Ro 7:2
IKo 11:3
Efe 5:22

c IKo 11:3
1Pe 3:1

Safu ya 2

a Kum 23:21

SURA YA 31

b Zb 94:1
Isa 1:24
Nah 1:2

c Hes 22:7
Hes 25:1-3
Hes 25:17,18
IKo 10:8
Ufu 2:14

d Hes 27:12,13
Kum 32:48-50

e Hes 26:51

f Hes 25:7,8

g Hes 10:2,9

ni ikiwa mume wake hampingi siku baada ya siku, basi amekubali viapo vyote au nadhiri zote za kujinyima za mke wake. Anakubaliana nazo kwa sababu hakumpinga siku alipomsikia akiweka nadhiri hizo. **15** Lakini mume wake akizifuta baadaye, baada ya siku aliyozisikia, atakuwa na hatia kwa kosa la mke wake.^a

16 "Hizo ndizo sheria ambazo* Yehova alimwamuru Musa kuhusu mume na mke wake, na kuhusu baba na binti yake anayeishi nyumbani kwa baba yake."

31 Kisha Yehova akamwambia Musa: **2** "Walipize kisasi^b Wamidiani^c kwa sababu ya mambo waliyowatendea Waisraeli. Baadaye utakufa na kuzikwa pamoja na watu wako."^d

3 Basi Musa akawaambia watu hivi: "Watarisheni wanaume wakapigane* na Wamidiani na kulipiza kisasi cha Yehova dhidi yao. **4** Mtapeleka jeshini wanaume 1,000 kutoka katika kila kabila la Israeli." **5** Kwa hiyo wanaume 1,000 kutoka katika kila kabila miongoni mwa maelfu ya Waisraeli,^e jumla ya wanaume 12,000, walitayarishwa kwa ajili ya vita.

6 Kisha Musa akawatuma vitani wanaume 1,000 kutoka katika kila kabila, wakiwa pamoja na Finehasi^f mwana wa kuhani Eleazari aliyebeba mkononi mwake vyombo vitakatifu na tarumbeta za kutangaza mwito.^g

30:16 *Au "Hayo ndiyo masharti ambayo." **31:2** *Tnn., "utakusanywa kwa watu wako." Huu ni msemu wa kishairi unaorejelea kifo. **31:3** *Au "Tayarisheni jeshi likapigane."

7 Walipigana na Wamidiani, kama Yehova alivyomwamuru Musa, wakawaua wanaume wote. 8 Miongoni mwa watu waliouawa kulikuwepo wafalme watano wa Midiani, yaani, Evi, Rekemu, Suri, Huru, na Reba. Pia, walimuua kwa upanga Balaamu^a mwana wa Beori. 9 Lakini Waisraeli waliwachukua mateka wanawake wa Midiani na watoto wao. Walichukua pia wanyama wao wote, naam, mifugo yao yote, na mali zao zote. 10 Waliteketeza majiji yote ambamo Wamidiani waliishi na kambi zao zote.* 11 Wakachukua nyara zote na mateka wote, wanadamu na wanyama. 12 Wakamletea Musa na kuhani Eleazari na Waisraeli wote mateka hao na nyara hizo kambini, katika jangwa tambarare la Moabu,^b karibu na Yordani huko Yeriko.

13 Kisha Musa na kuhani Eleazari na wakuu wote wa Waisraeli wakatoka ili kukutana nao nje ya kambi. 14 Lakini Musa alikasirishwa sana na wanaume waliowekwa kusimamia jeshi, yaani, wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia waliokuwa wakirudi kutoka vitani. 15 Musa akawauliza: “Kwa nini mmewaacha hai wanawake wote? 16 Kumbukeni kwamba hao ndio waliochochewa na Balaamu kuwashawishi Waisraeli wakose uaminifu^c kwa Yehova kule Peori,^d na kuwaletea pigo watu wa Yehova.^e 17 Sasa muueni kila mtoto wa kiume na kila mwanamke ambaye amewahi kufanya ngono na mwanamume. 18 Lakini msiwaue wa-

31:10 *Au “kambi zao zote zilizozingirwa na kuta.”

SURA YA 31

a Hes 22:12
2Pe 2:15
Ufu 2:14

b Hes 22:1

c Hes 25:1, 2
Ufu 2:14

d Hes 25:17, 18
Kum 4:3
Yos 22:17

e Hes 25:9
1Ko 10:8

Safu ya 2

a Hes 31:35

b Hes 5:2
Hes 19:11, 16

c Hes 19:20

d Hes 19:9

e Hes 19:19, 20

sichana wote ambao hawajawahi kufanya ngono na mwanamume.^a 19 Nanyi mnapaswa kupiga kambi nje ya kambi kwa siku saba. Kila mtu miongoni mwenu ambaye amemuua mtu na kila mtu ambaye amemgusa mtu aliyeuawa^b anapaswa kujitakasa^c siku ya tatu na siku ya saba, ninyi na mateka wenu. 20 Mnapaswa pia kutakasa kutokana na dhambi kila vazi, kila kitu kilichotengenezwa kwa ngozi, kila kitu kilichotengenezwa kwa manyoya ya mbuzi, na kila kitu kilichotengenezwa kwa mbao.”

21 Ndipo kuhani Eleazari akawaambia wanaume walioenda vitani: “Hii ndiyo sheria ambayo Yehova amempa Musa, 22 ‘Ni dhahabu, fedha, shaba, chuma, bati, na madini ya risasi tu, 23 yaani, kila kitu kinachoweza kustahimili moto, ndicho mnapaswa kupitisha motoni, nacho kitakuwa safi. Hata hivyo, kinapaswa pia kusafishwa kwa maji ya kutakasa.^d Kila kitu ambacho hakivezi kustahimili moto, mnapaswa kukitakasa kwa maji. 24 Nanyi mnapaswa kufua mavazi yenu siku ya saba na kuwa safi, kisha mnaweza kuingia kambini.’”^e

25 Tena Yehova akamwambia Musa hivi: 26 “Wewe pamoja na kuhani Eleazari na viongozi wa koo* za Waisraeli hesabuni nyara zote, kutia ndani wanadamu na wanyama waliotekwa. 27 Gaweni nyara hizo katika mafungu mawili, ili wanajeshi walioenda vitani wapate fungu moja na

31:26 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

Waisraeli wengine fungu lingine.^a **28** Kutoka kwa wanajeshi walioenda vitani, mtachukua nafsi* moja kutoka kwa kila nafsi 500 za wanadamu, za ng'ombe, za punda, na kondoo ili iwe kodi ya Yehova. **29** Mnapaswa kuchukua nafsi hizo kutoka katika fungu lao na kumpa kuhani Eleazari kama mchango kwa Yehova.^b **30** Kutoka katika fungu ambalo Waisraeli watapewa, mnapaswa kuchukua nafsi moja kutoka kwa kila nafsi 50 za wanadamu, za ng'ombe, za punda, za kondoo, na za kila aina ya mnyama wa kufugwa, na kuwapa Walawi,^c wanaotimiza majukumu katika hema la Yehova la ibada."^d

31 Basi Musa na kuhani Eleazari wakafanya kama Yehova alivyomwamuru Musa. **32** Nyara na vitu vyote ambavyo watu walichukua vitani ni kondoo 675,000, **33** ng'ombe 72,000, **34** na punda 61,000. **35** Wanawake ambao hawakuwa wamefanya ngono na mwanamume^e walikuwa wanawake* 32,000. **36** Na nusu iliyo kuwa fungu la wale walioenda vitani ilikuwa kondoo 337,500. **37** Kondoo 675 kati yao walichukuliwa ili kuwa kodi kwa Yehova. **38** Pia, kulikuwa na ng'ombe 36,000, na ng'ombe 72 kati yao walichukuliwa ili kuwa kodi kwa Yehova. **39** Punda walikuwa 30,500, na punda 61 kati yao walichukuliwa ili kuwa kodi kwa Yehova. **40** Wanadamu walikuwa 16,000, na 32 kati yao walichukuliwa ili kuwa kodi kwa Yehova. **41** Kisha Musa akampa

31:28 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
31:35 *Au "nafsi."

SURA YA 31

a Yos 22:7, 8
1Sa 30:24

b Hes 18:20, 29

c Kum 12:19

d Hes 3:6, 7
Hes 18:2, 3
1Nya 23:32

e Hes 31:18

Safu ya 2

a Hes 18:8, 19

b Kum 12:19

c Hes 3:6, 7
Hes 18:2, 3
1Nya 23:32

d Hes 31:4

e Kut 23:27
Law 26:7, 8

kuhani Eleazari kodi hiyo iwe mchango wa Yehova,^a kama Yehova alivyomwamuru Musa.

42 Ile nusu waliyopewa Waisraeli ambayo Musa aliitenga na nusu waliyopewa wanajeshi walioenda vitani, **43** ilikuwa kondoo 337,500, **44** ng'ombe 36,000, **45** punda 30,500, **46** na wanadamu 16,000. **47** Kisha kutoka katika nusu hiyo ambayo ni fungu la Waisraeli, Musa alichukua nafsi moja kutoka kwa kila nafsi 50 za wanadamu na za wanyama akawapa Walawi^b waliotimiza majukumu katika hema la Yehova la ibada,^c kama Yehova alivyomwamuru Musa.

48 Kisha wanaume walioyekwa kusimamia maelfu ya wanajeshi,^d yaani, wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia, wakamfikia Musa, **49** na kumwambia: "Sisi watumishi wako tumewahesabu wanajeshi walio chini ya usimamizi wetu, na hakuna hata mmoja wao anayekosekana.^e **50** Kwa hiyo mruhusu kila mmoja wetu atoe vitu alivyopata ili viwe vya Yehova, yaani, vitu vya dhahabu, mikufu ya miguuni, bangili, pete za muhuri, vipuli, na vito vingine, ili Yehova afunike dhambi zetu."

51 Basi Musa na kuhani Eleazari wakapokea dhahabu hiyo kutoka kwao, naam, vito vyote. **52** Dhahabu yote ambayo wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia walimtolea Yehova mchango ilikuwa shekeli 16,750.* **53** Kila wanajeshi alikuwa amejichukulia

31:52 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

nyara. **54** Musa na kuhani Eleazari walipokea dhahabu hiyo kutoka kwa wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia na kuleta katika hema la mkutano ili iwe kumbukumbu mbele za Yehova kwa ajili ya Waisraeli.

32 Sasa wana wa Rubeni^a na wana wa Gadi^b wali-kuwa na mifugo mingi sana, wakaona kwamba eneo la Yazeri^c na eneo la Gileadi yalikuwa maeneo mazuri kwa mifugo. **2** Basi wana wa Gadi na wana wa Rubeni wakaja kwa Musa, kuhani Eleazari, na wakuu wa Waisraeli na kuwaambia hivi: **3** “Atarothi, Diboni, Yazeri, Nimra, Heshboni,^d Eleale, Sebam, Nebo,^e na Beoni,^f **4** maeneo ambayo Yehova aliyashinda mbele ya Waisraeli,^g ni maeneo mazuri kwa mifugo, nasi watumishi wenu tuna mifugo mingi.”^h **5** Wakaendelea kusema, “Ikiwa sisi watumishi wenu tumepata kibali machoni penu, tupeni maeneo haya tuyamiliki. Msituvushe ng’ambo ya Mto Yordani.”

6 Lakini Musa akawaambia hivi wana wa Gadi na wana wa Rubeni: “Je, ndugu zenu wataenda vitani huku ninyi mkiendelea kukaa hapa? **7** Kwa nini muwavunje moyo Waisraeli wasivuke kuingia katika nchi ambayo kwa hakika Yehova atawapa? **8** Hivyo ndivyo baba zenu walivyofanya nilipowatuma kutoka Kadeshbarnea wakaione ile nchi.ⁱ **9** Walipofika kwenye Bonde la Eshkoli^j na kuiona nchi hiyo, waliwavunja moyo Waisraeli wasiingie katika nchi ambayo Yehova angewapa.^k **10** Yehova aliwaka hasira siku

SURA YA 32

a Hes 26:7

b Hes 26:18

c Hes 21:32

d Hes 21:26

e Hes 33:47

f Hes 32:37,38

g Hes 21:23,24
Kum 2:24

h Kum 2:35

i Hes 13:31
Yos 14:7,8

j Hes 13:23
Kum 1:24

k Hes 13:32
Kum 1:26-28

Safu ya 2

a Zb 95:11
Eze 20:15
Ebr 3:18

b Hes 14:29,30
Kum 2:14

c Mwa 13:14,15
Mwa 26:3
Mwa 28:13

d Hes 13:30

e Yos 19:49

f Hes 14:24
Kum 1:34-38
Yos 14:8

g Hes 14:33
Kum 29:5
Yos 5:6
Zb 95:10
Mdo 13:18

h Hes 26:63,64
Kum 2:14
1Ko 10:5
Ebr 3:17

i Kum 3:18
Yos 4:12

j Yos 22:1,4

hiyo na kuapa hivi:^a **11** ‘Wanaume waliotoka Misri wenyewe umri wa kuanzia miaka 20 na zaidi hawataiona nchi^b ambayo niliapa kwamba nitampa Abrahamu, Isaka, na Yakobo,^c kwa sababu hawakunifuata kwa moyo wote—**12** isipokuwa Kalebu^d mwana wa Yefune, Mkenizi, na Yohshua^e mwana wa Nuni, kwa sababu wamenifuata mimi Yehova kwa moyo wote.’^f **13** Basi hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Waisraeli naye akawafanya watangetange nyikani kwa miaka 40,^g mpaka kizazi chothe kilichokuwa kikifanya maovu machoni pa Yehova kilipoangamia.^h **14** Na sasa ninyi mmekuwa kama baba zenu, kundi la watenda dhambi wanaozidisha hasira kali ya Yehova dhidi ya Waisraeli. **15** Mkigeuka na kuacha kumfuata, kwa hakika atawaacha tena watu hawa nyikani, nanyi mtasababisha watu hawa wote waangamizwe.”

16 Baadaye wakaja tena kwake na kumwambia: “Turuhusu tujenge hapa mazizi ya mawe kwa ajili ya mifugo yetu na majiji kwa ajili ya watoto wetu. **17** Lakini sisi tutaeendelea kuwa tayari kwa ajili ya vitaⁱ na tutakuwa mstari wa mbele mpaka tutakapowafikisha Waisraeli mahali pao, wakati huo watoto wetu watakaa katika majiji yenye ngome, wakiwa salama kutoka kwa wakaaji wa nchi. **18** Hatutarudi katika nyumba zetu mpaka kila Mwisraeli atakaporithi eneo lake.^j **19** Kwa maana hatutapokea urithi wote pamoja nao katika eneo lote lililo ng’ambo ya Yordani, kwa sababu tumepokea urithi

wetu upande wa mashariki wa Yordani.”^a

20 Musa akawaambia: “Ikiwa mtafanya hivi: Ikiwa mtachukua silaha mbele za Yehova kwa ajili ya vita;^b **21** na ikiwa kila mmoja wenu atachukua silaha na kuvuka Yordani mbele za Yehova anapowafukuza maadui wake kutoka mbele zake^c **22** mpaka mtakaposhinda na kuichukua nchi mbele za Yehova,^d mna-weza kurudi^e nanyi hamtakuwa na hatia mbele za Yehova na Waisraeli. Ndipo Yehova atakapokubali mmiliki nchi hii.^f **23** Lakini msipofanya hivyo, mtakuwa mmemtendea dhambi Yehova. Nanyi mjue kwamba mtaadhibiwa kwa sababu ya dhambi yenu. **24** Kwa hiyo mnaweza kujenga majiji kwa ajili ya watoto wenu na mazizi kwa ajili ya mifugo yenu,^g lakini ni lazima mfanye mambo mliyoahidi.”

25 Wana wa Gadi na wana wa Rubeni wakamwambia Musa hivi: “Bwana wetu, sisi watumishi wako tutafanya kama unavyotuamuru. **26** Watoto wetu, wake zetu, mifugo yetu, na wanyama wetu wote watabaki hapa katika majiji ya Gileadi,^h **27** lakini sisi watumishi wako tutavuka, kila mwanamume aliyechukua silaha ili kupigana vita mbele za Yehova,ⁱ kama unavyosema bwana wetu.”

28 Basi Musa akampa kuhani Eleazari, Yoshua mwana wa Nuni, na viongozi wa koo* za makabila ya Waisraeli amri kuwahusu. **29** Musa akawaambia hivi: “Ikiwa wana wa Gadi na wana wa Rubeni

SURA YA 32

a Hes 32:33
Yos 12:1
Yos 13:8

b Yos 4:13

c Zb 78:55

d Yos 11:23
Yos 18:1
Zb 44:2

e Yos 22:4, 9

f Kum 3:19, 20
Yos 1:14, 15
Yos 13:8

g Hes 32:16
Hes 32:34-38

h Yos 1:12-14

i Yos 4:12

Safu ya 2

a Yos 13:15, 24

b Yos 4:13

c Kum 3:12

d Yos 22:7

e Hes 21:23, 24
Kum 2:31

f Kum 3:4

g Hes 33:45
Yos 13:15, 17

h Hes 32:3, 4

i Kum 2:36
Yos 12:1, 2

j Hes 21:32

k Amu 8:11

l Hes 32:3, 4

m Yos 13:27, 28

n Hes 21:26

o Hes 32:3, 4

p Yos 13:15, 19

q Hes 32:3, 4

r Yos 13:15, 17

s Hes 26:29

watavuka Yordani pamoja nanyi, yaani, kila mwanamume aliyechukua silaha ili kupigana vita mbele za Yehova, nanyi mshinde na kuchukua eneo hilo, basi mtawapa eneo la Gileadi ili walimiliki.^a **30** Lakini ikiwa hawatachukua silaha na kuvuka pamoja nanyi, basi wataishi pamoja nanyi katika nchi ya Kanaani.”

31 Basi wana wa Gadi na wana wa Rubeni wakajibu: “Sisi watumishi wako tutafanya mambo ambayo Yehova ametuambia. **32** Tutachukua silaha na kuvuka mbele za Yehova kuingia nchi ya Kanaani,^b lakini urithi wetu utakuwa upande huu wa Yordani.” **33** Hivyo Musa akawapa—wana wa Gadi, wana wa Rubeni,^c na nusu ya kabila la Manase^d mwana wa Yosefu—ufalme wa Sihoni^e mfalme wa Waamori na ufalme wa Ogu^f mfalme wa Bashani, maeneo hayo na majiji yaliyokuwemo na pia majiji jirani.

34 Wana wa Gadi wakajenga* Diboni,^g Atarothi,^h Aroeri,ⁱ **35** Atroth-shofani, Yazeri,^j Yogbeha,^k **36** Bethnimra,^l Beth-harani,^m majiji yenye ngome, na mazizi ya mawe kwa ajili ya mifugo. **37** Nao wana wa Rubeni wakajenga Heshboni,ⁿ Eleale,^o Kiriathaimu,^p **38** Nebo,^q na Baal-meoni—majina ya majiji hayo yalibadilishwa—na Sibma; nao wakaanza kuyapa majina mapya majiji waliyojenganya upya.

39 Wana wa Makiri^s mwana wa Manase walishambulia eneo la Gileadi, wakaliteka, na kuwafukuza Waamori

32:28 * Yaani, ukoo wa upande wa baba.

32:34 * Au “wakajenga upya.”

waliokaa humo. **40** Kwa hiyo Musa akampa Makiri mwana wa Manase, Gileadi, akaanza kukaa katika eneo hilo.^a

41 Na Yairi mwana wa Manase akawashambulia wakaaji wa eneo hilo na kuteka vijiji vyao vya mahema, akavii-ta Hawoth-yairi.^{*b} **42** Naye Noba akashambulia na kuliteka jiji la Kenathi na miji yake, naye akalita Noba, jina lake mwenyewe.

33 Waisraeli walipiga kambi katika vituo vifuatavyo walipotoka nchini Misri^c kulingana na vikosi vyao^{*d} wakiongozwa na Musa na Haruni.^e **2** Musa aliandika kila kituo katika safari yao kama Yehova alivyomwagiza, na hivi ndivyo vituo vya safari yao, kituo baada ya kituo.^f **3** Waliondoka Ramesesi^g siku ya 15 ya mwezi wa kwanza.^h Siku hiyohiyo baada ya Pasaka,ⁱ Waisraeli waliondoka kwa ujasiri* huku Wamisri wote wakiwatazama. **4** Wakati huo, Wamisri walikuwa wakiwazika wazaliwa wao wote wa kwanza ambao Yehova aliwaangamiza,^j kwa kuwa Yehova alikuwa ameteteleza hukumu dhidi ya miungu yao.^k

5 Kwa hiyo Waisraeli wakaondoka Ramesesi na kupiga kambi Sukothi.^l **6** Kisha wakaondoka Sukothi na kupiga kambi Ethamu,^m kwenye ukingo wa nyika. **7** Halafu wakaondoka Ethamu, waka-geuka na kurudi Pihahirothi, mbele ya Baal-sefoni,ⁿ wakapiga kambi karibu na Migdoli.^o **8** Kisha wakaondoka Pihahirothi na kupita kati-

32:41 *Maana yake "Vijiji vya Mahema vya Yairi." 33:1 *Tnn., "majeshi yao." 33:3 *Tnn., "mkono ulioinuliwa."

SURA YA 32

a Kum 3:13
Yos 13:31
Yos 17:1

b Kum 3:14
Yos 13:29, 30

SURA YA 33

c Kut 12:51

d Kut 13:18

e Yos 24:5
1Sa 12:8

f Hes 9:17

g Mwa 47:11
Kut 12:37

h Kut 12:2
Kut 13:4

i Kut 12:3, 6
Kum 16:1

j Kut 12:29
Zb 78:51

k Kut 12:12
Kut 18:11

l Kut 12:37

m Kut 13:20

n Kut 14:9

o Kut 14:2

Safu ya 2

a Kut 14:22

b Kut 15:22

c Kut 13:20

d Kut 15:23

e Kut 15:27

f Kut 16:1

g Kut 17:1, 8

h Kut 18:5
Kut 19:1, 2
Hes 1:1
Hes 3:4
Hes 9:1

i Hes 11:34
Kum 9:22

j Hes 11:35
Hes 12:16

kati ya bahari^a mpaka nyikani,^b wakaendelea kusafiri kwa siku tatu katika nyika ya Ethamu^c na kupiga kambi huko Mara.^d

9 Kisha wakaondoka Mara na kufika Elimu. Huko Elimu kulikuwa na chemchemi 12 za maji na mitende 70, kwa hiyo wakapiga kambi mahali hapo.^e

10 Halafu wakaondoka Elimu na kupiga kambi kando ya Bahari Nyekundu. **11** Kisha wakaondoka kando ya Bahari Nyekundu na kupiga kambi katika nyika ya Sini.^f

12 Halafu wakaondoka katika nyika ya Sini na kupiga kambi Dofka. **13** Baadaye wakaondoka Dofka na kupiga kambi Alushi. **14** Kisha wakaondoka Alushi na kupiga kambi Refidimu,^g ambapo hapakuwa na maji ya kunywa. **15** Halafu wakaondoka Refidimu na kupiga kambi katika nyika ya Sinai.^h

16 Wakaondoka katika nyika ya Sinai na kupiga kambi Kibroth-hataava.ⁱ **17** Kisha wakaondoka Kibroth-hataava na kupiga kambi Haserothi.^j

18 Baada ya hapo wakaondoka Haserothi na kupiga kambi Rithma. **19** Kisha wakaondoka Rithma na kupiga kambi Rimon-peresi. **20** Halafu wakaondoka Rimon-peresi na kupiga kambi Libna. **21** Wakaondoka Libna na kupiga kambi Risa. **22** Kisha wakaondoka Risa na kupiga kambi Kehelatha. **23** Halafu wakaondoka Kehelatha na kupiga kambi kwenye Mlima Sheferi.

24 Kisha wakaondoka kwenye Mlima Sheferi na kupiga kambi Harada. **25** Halafu wakaondoka Harada

na kupiga kambi Makelothi. **26** Kisha wakaondoka^a Makelothi na kupiga kambi Tahathi. **27** Halafu wakaoondoka Tahathi na kupiga kambi Tera. **28** Kisha wakaoondoka Tera na kupiga kambi Mithka. **29** Baadaye wakaoondoka Mithka na kupiga kambi Hashmona. **30** Kisha wakaoondoka Hashmona na kupiga kambi Moserothi. **31** Halafu wakaondoka Moserothi na kupiga kambi Bene-yaakani.^b **32** Kisha wakaondoka Bene-yaakani na kupiga kambi Hor-hagidgadi. **33** Halafu wakaoondoka Hor-hagidgadi na kupiga kambi Yotbata.^c **34** Baadaye wakaondoka Yotbata na kupiga kambi Abrona. **35** Kisha wakaondoka Abrona na kupiga kambi Esion-geberi.^d **36** Kisha wakaondoka Esion-geberi na kupiga kambi katika nyika ya Zini,^e yaani, Kadeshi. **37** Baadaye wakaondoka Kadeshi na kupiga kambi kwenye Mlima Hori,^f mpakani mwa nchi ya Edomu. **38** Kisha kuhani Haruni akapanda juu ya Mlima Hori kwa agizo la Yehova, akafa huko siku ya kwanza ya mwezi wa tano, mwaka wa 40 tangu Waisraeli walipotoka nchini Misri.^g **39** Haruni alikuwa na umri wa miaka 123 alipokufa juu ya Mlima Hori.

40 Basi mfalme wa Aradi,^h Mkanaani, aliyekuwa akiishi Negebu katika nchi ya Kanaani, akasikia kwamba Waisraeli wanakuja.

41 Baada ya muda wakaoondoka kwenye Mlima Horiⁱ na kupiga kambi Salmona. **42** Kisha wakaondoka Salmona na kupiga kambi Punoni. **43** Halafu wakaondoka Pu-

SURA YA 33

a Hes 9:17

b Kum 10:6

c Kum 10:7

d Kum 2:8
1Fa 9:26e Hes 20:1
Hes 27:14
Kum 32:51
Yos 15:1

f Hes 20:22

g Kum 10:6

h Hes 21:1

i Hes 21:4

Safu ya 2

a Hes 21:10

b Mwa 19:36, 37
Hes 21:11, 13

c Hes 32:34

d Hes 27:12
Kum 32:48, 49

e Kum 34:1

f Hes 22:1

g Hes 25:1
Yos 2:1

h Yos 3:17

i Law 26:1

j Law 19:4
Kum 27:15k Kut 23:24
Kut 34:13, 17
Kum 7:5
Kum 12:3

l Kum 32:8

m Met 16:33

n Hes 26:53, 54

noni na kupiga kambi Obothi.^a **44** Wakaondoka Obothi na kupiga kambi Iye-abarimu kwenye mpaka wa Moabu.^b **45** Baadaye wakaondoka Iyimu* na kupiga kambi Dibongadi.^c **46** Kisha wakaondoka Dibongadi na kupiga kambi Almon-diblathaimu. **47** Halafu wakaondoka Almon-diblathaimu na kupiga kambi kwenye milima ya Abarimu^d karibu na Nebo.^e **48** Mwishowe wakaondoka kwenye milima ya Abarimu na kupiga kambi katika jangwa tambarare la Moabu karibu na Yordani huko Yeriko.^f **49** Wakaoondoka kupiga kambi kandokando ya Mto Yordani kuanzia Beth-yeshimothi mpaka Abelshtimtu,^g katika jangwa tambarare la Moabu.

50 Yehova akazungumza na Musa katika jangwa tambarare la Moabu karibu na Yordani huko Yeriko, akamwambia: **51** "Waambie hivi Waisraeli: 'Mnavuka Mto Yordani kuingia katika nchi ya Kanaani.^h **52** Ni lazima muwafukuzze wakaaji wote wa nchi hiyo kutoka mbele yenu na kuharibu sanamu zao zote za maweⁱ na sanamu zao zote za chuma,^{*j} nanyi mnapaswa kuharibu mahali pao pote patakati-fu palipo juu.^k **53** Mtamiliki nchi hiyo na kuishi humo, kwa maana hakika nitawapa nchi hiyo ili mwimiliki.^l **54** Mtai-gawanya nchi hiyo kwa kura^m na kuimiliki kulingana na familia zenu. Kundi kubwa litapokea urithi mkubwa zaidi na kikundi kidogo kitapokea urithi mdogo.ⁿ Kila mtu atapokea urithi wake mahali

33:45 *Huu ni ufupisho wa Iye-abarimu. **33:52** *Tnn., "za kuyeyushwa."

ambapo kura yake itaangukia. Mtapokea urithi wenu wa nchi kulingana na makabila ya baba zenu.^a

55 “Hata hivyo, msipowafukuza wakaaji wa nchi hiyo kutoka mbele yenu,^b basi wale mtakaoruhusu wabaki watakuwa kama vibanzi katika macho yenu na kama miiba kwenye mbavu zenu, nao watawasumbua katika nchi mtakayoiishi.^c **56** Nami nitawatendea ninyi mambo niliyokusudia kuwatendea wao.”^d

34 Jehova akaendelea kumwambia Musa: **2** “Wape Waisraeli maagizo haya: ‘Mta- kapoingia katika nchi ya Kanaani,^e nchi mtakayoirithi, hii ndiyo itakayokuwa mipaka ya nchi hiyo ya Kanaani.’^f

3 “Mpaka wenu wa kusini utaanzia nyika ya Zini kando ya Edomu, na upande wa mashariki mpaka huo wa kusini utaanzia mwisho wa Bahari ya Chumvi.^g **4** Kisha mpaka huo utapinda na kwenda upande wa kusini wa mwinuko wa Akrabimu,^h nao utae- ndelea mpaka Zini na kuishia upande wa kusini wa Kadeshbarnea.ⁱ Kisha utaenda Hasaradari^j na kuendelea mpaka Asimoni. **5** Mpaka huo utapinda huko Asimoni na kuelekea kwenye Bonde la Misri na kuishia kwenye Bahari ya Mediterania.^k

6 “Mpaka wenu wa magharibi utakuwa Bahari Kuu* na pwani. Huo utakuwa mpaka wenu wa magharibi.^l

7 “Huu ndio utakaokuwa mpaka wenu wa kaskazini: Mtaweka alama kuanzia

34:6 *Yaani, Mediterania.

SURA YA 33

a Yos 15:1
Yos 16:1
Yos 18:11

b Amu 1:21
Zb 106:34

c Kut 23:31-33
Kum 7:3, 4
Yos 23:12, 13
Amu 2:2, 3

d Law 18:28
Yos 23:15

SURA YA 34

e Mwa 15:18
Mwa 17:6

f Mwa 10:19
Kum 4:38
Yos 1:4
Yos 14:1
Yer 3:19
Mdo 17:26

g Yos 15:1, 2

h Amu 1:36

i Hes 13:26
Hes 32:8

j Yos 15:1, 3

k Kut 23:31
Yos 15:1, 4

l Yos 1:4
Yos 15:12

Safu ya 2

a Hes 33:37
Kum 32:50

b Hes 13:21
2Fa 14:25

c Eze 47:15

d Eze 47:17

e Kum 3:16, 17
Yos 11:1, 2
Lu 5:1
Yoh 6:1

f Yos 15:1, 2

g Kum 8:7-9

h Hes 26:55
Hes 33:54
Yos 14:2
Yos 18:6
Met 16:33

i Hes 32:33

Kum 3:12, 13
Yos 13:8

j Hes 32:5, 32

k Hes 3:32
Hes 20:26
Yos 14:1

l Hes 14:38
Hes 27:18
Yos 19:51

Bahari Kuu mpaka Mlima Hori.^a **8** Kutoka Mlima Hori mtaweka alama mpaka Lebohamathi,^{*b} nao utaishia Sedadi.^c **9** Kisha utaendelea hadi Zifroni na kuishia Hasarenani.^d Huo utakuwa mpaka wenu wa kaskazini.

10 “Kisha mtaweka alama ya mpaka wenu wa mashariki kuanzia Hasarenani hadi Shefamu. **11** Mpaka huo utaanzia Shefamu hadi Ribla, upande wa mashariki wa Aini, nao utashuka na kuvuka mteremko wa mashariki wa Bahari ya Kinerethi.^{*e} **12** Kisha utaendelea mpaka Yordani na kuishia kwenye Bahari ya Chumvi.^f Hiyo ndiyo itakayokuwa nchi yenu^g na mipaka inayoizunguka.”

13 Kwa hiyo Musa akawapa Waisraeli maagizo haya: “Hiyo ndiyo nchi mtakayoigawanya kwa kura na kuimiliki,^h kama Jehova alivyoamuru kwamba makabila tisa na nusu yape- we nchi hiyo. **14** Kwa maana kabila la Rubeni kulingana na koo zao,^{*} kabila la Gadi kulingana na koo zao,^{*} na nusu ya kabila la Manase tayari yamechukua urithi wao.ⁱ **15** Makabila hayo mawili na nusu tayari yamechukua urithi wao upande wa mashariki wa Yordani karibu na Yeriko, upande wa mapambazuko ya jua.”^j

16 Jehova akaendelea kumwambia Musa, **17** “Haya ndiyo majina ya wanaume watakaowagawia nchi ili mwimiliki: kuhani Eleazari^k na Yohshua^l mwana wa Nuni. **18** Nanyi mtachukua mkuu mmo-

34:8 *Au “njia ya kuingia Hamathi.”

34:11 *Yaani, ziwa la Genesareti, au Bahari ya Galilaya. **34:14** *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

ja kutoka katika kila kabila ili awasaidie kuigawanya nchi mtakayorithi.^a **19** Haya ndiyo majina ya wanaume hao: kutoka kabila la Yuda,^b Kalebu^c mwana wa Yefune; **20** kutoka kabila la wana wa Simeoni,^d Shemueli mwana wa Amihudi; **21** kutoka kabila la Benjamini,^e Elidadi mwana wa Kisloni; **22** kutoka kabila la wana wa Dani,^f mkuu mmoja, Buki mwana wa Yogli; **23** kutoka kwa wana wa Yosefu,^g kwa ajili ya kabila la wana wa Manase,^h mkuu mmoja, Hanieleli mwana wa Efodi; **24** kutoka kabila la wana wa Efraimu,ⁱ mkuu mmoja, Kemueli mwana wa Shiftani; **25** kutoka kabila la wana wa Zabuloni,^j mkuu mmoja, Elisafani mwana wa Parnaki; **26** kutoka kabila la wana wa Isakari,^k mkuu mmoja, Paltieli mwana wa Azani; **27** kutoka kabila la wana wa Asheri,^l mkuu mmoja, Ahihudi mwana wa Shelomi, **28** na kutoka kabila la wana wa Nafatali,^m mkuu mmoja, Pedaheli mwana wa Amihudi.” **29** Hando ndio wanaume ambao Yehova aliamuru wawagawie Waisraeli ardhi katika nchi ya Kanaani.ⁿ

35 Yehova akaendelea kuzungumza na Musa katika jangwa tambarare la Moabu karibu na Yordani^o huko Yeriko, akamwambia: **2** “Waagize Waisraeli wawape Walawi majiji ya kuishi kutoka katika urithi watakaomiliki,^p nao wanapaswa kuwapa Walawi malisho yanayozunguka majiji hayo.^q **3** Wataishi katika majiji hayo, na malisho hayo yatakuwa ya mifugo yao, na ya mali zao, na wanya-

SURA YA 34

a Hes 1:4, 16

b Yos 15:1

c Hes 14:30
Hes 26:65

d Yos 19:1

e Yos 18:11

f Yos 19:40

g Mwa 46:20
Mwa 48:5
Yos 16:1

h Yos 17:1

i Yos 16:5

j Yos 19:10

k Yos 19:17

l Yos 19:24

m Yos 19:32

n Hes 34:18
Kum 32:8
Yos 19:51
Mdo 17:26

SURA YA 35

o Hes 22:1
Hes 36:13p Mwa 49:7
Kum 18:1
Yos 14:4q Law 25:32-34
Yos 21:3
2Nya 11:14

Safu ya 2

a Yos 20:2, 3,
7, 8
Yos 21:13, 21,
27, 32, 36, 38

b Kum 4:42

c Yos 21:3

d Mwa 49:7

e Hes 26:54
Hes 33:54f Kut 3:8
Kut 23:23
Hes 34:2g Kut 21:12, 13
Kum 4:42
Kum 19:4, 5h Hes 35:19
Kum 19:6

ma wao wengine wote. **4** Malisho ya majiji mtakayowapa Walawi yatakuwa na upana wa mikono 1,000* kila upande kutoka kwenye ukuta wa jiji. **5** Mtapima nje ya jiji mikono 2,000 upande wa mashariki, mikono 2,000 upande wa kusini, mikono 2,000 upande wa magharibi, na mikono 2,000 upande wa kaskazini; jiji litakuwa katikati. Hayo ndiyo yatakatayokuwa malisho ya majiji yao.

6 “Majiji mtakayowapa Walawi yatakuwa majiji 6 ya makimbilio^a ili mtu anayemuua mwenzake akimbilie humo,^b pia mtawapa majiji mengi ne 42. **7** Mtapawa Walawi jumla ya majiji 48 pamoja na malisho yake.^c **8** Majiji mtakayowapa yatatoka katika urithi wa Waisraeli.^d Mtachukua majiji mengi kutoka kwa makabila makubwa na majiji machache kutoka kwa makabila madogo.^e Kila kabila litawapa Walawi baadhi ya majiji yake kulingana na urithi ambao litapokea.”

9 Yehova akaendelea kumwambia Musa, **10** “Waaambia hivi Waisraeli: ‘Mnavuka Mto Yordani kuingia katika nchi ya Kanaani.’ **11** Mnapaswa kuchagua majiji yatakayowafaa ninyi ili yawe majiji ya makimbilio ili mtu anayemuua mwenzake bila kukusudia akimbilie humo.^g **12** Majiji hayo yatakuwa mahali penu pa kukimbilia kutoka kwa mtu anayelipiza kisasi cha damu,^h ili muajaji asiuawe kabla ya kesi yake kusikilizwa

35:4 * Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

mbele ya kusanyiko.^a **13** Majiji sita ya makimbilio mtakayotoa yatatumiwa kwa kusu-di hilo. **14** Mtatoa majiji matatu upande huu wa Yordani^b na majiji matatu katika nchi ya Kanaani^c ili yawe majiji ya makimbilio. **15** Majiji hayo sita yatakuwa majiji ya makimbilio kwa ajili ya Waisraeli, kwa ajili ya wageni,^d na kwa ajili ya wahamiaji wanaoishi miongoni mweni, ili mtu yeyote anayemuua mwenzake bila kukusudia akimbilie humo.^e

16 “Lakini ikiwa mtu amempiga mwenzake kwa kifaa cha chuma na kumuua, yeye ni muuaji. Lazima muuaji huyo auawe.^f **17** Ikiwa alimpiga kwa jiwe ambalo lina-weza kuuu, na mtu huyo akafa, aliyempiga ni muuaji. Lazima muuaji huyo auawe. **18** Ikiwa alimpiga kwa kifaa cha mbao kinachoweza kuuu, na mtu huyo akafa, aliyempiga ni muuaji. Lazima muuaji huyo auawe.

19 “Mwenye kulipiza kisasi cha damu ndiye atakayemuua muuaji. Atakapokutana naye, atamuua yeye mwenyewe. **20** Ikiwa mtu anayemchukia mwenzake anamsukuma au kumtupia kitu fulani kwa nia mbaya* na kumuua,^g **21** au kwa sababu ya chuki anampiga kwa mkono na kumuua, ni lazima mtu huyo aliyempiga auawe. Yeye ni muuaji. Mtu anayelipiza kisasi cha damu atamuua muuaji huyo atakapokutana naye.

22 “Lakini ikiwa alimsukuma au kumtupia kitu chochote na kumuua bila kukusudia

35:20 *Tnn., “huku akimvizia.”

SURA YA 35

a Kum 19:11, 12
Yos 20:5, 9

b Kum 4:41-43

c Kum 19:8, 9
Yos 20:7

d Kut 12:49
Law 19:34
Hes 15:16

e Yos 20:2, 3

f Mwa 9:5
Kut 21:12
Law 24:17
Kum 19:11, 12

g Kut 21:14
Kum 19:11, 12

Safu ya 2

a Kut 21:12, 13
Kum 19:4, 5
Yos 20:2, 3

b Hes 35:12
Yos 20:4, 5

c Kut 29:4, 7

d Yos 20:6

e Mwa 9:6
Kut 20:13

f Kum 17:6
Kum 19:15
Ebr 10:28

au bila chuki na bila nia mba-ya,^{*a} **23** au ikiwa alimwanguشيا jiwe bila kumwona na mtu huyo akafa, lakini hakuwa adui yake au hakukusudia kumduru, **24** basi watu wanapaswa kuhukumu kati ya muuaji na mtu anayelipiza kisasi cha damu, kwa kufuata sheria hizo.^b **25** Kisha watu watamwoko muuaji kutoka mikononi mwa mtu anayelipiza kisasi cha damu na kumrudisha katika jiji lake la makimbilio alimokuwa amekimbilia, naye atakaa humo mpaka kuhani mkuu aliyetiwa mafuta matakatifu^c atakapokufa.

26 “Lakini muuaji akitoka nje ya mpaka wa jiji la makimbilio alimokimbilia, **27** kisha mtu anayelipiza kisasi cha damu ampate nje ya mpaka wa jiji la makimbilio na kumuua, mtu huyo anayelipiza kisasi cha damu hatakuwa na hatia ya damu. **28** Kwa maana ni lazima muuaji akae katika jiji lake la makimbilio mpaka kuhani mkuu atakapokufa. Lakini baada ya kuhani mkuu kufa, muuaji anaweza kurudi katika ardhini anayomiliki.^d **29** Mtatumia sheria hizo kuhukumu katika vizazi vyenu vyote mahali popote mnapoishi.

30 “Yeyote anayemuua mtu* anapaswa kuuawa kama muuaji^e ikiwa kuna ushahidi kutoka kwa mashahidi;^f lakini hakuna mtu atakayeuawa[#] kwa ushahidi wa mtu mmoja tu. **31** Hampaswi kuchukua fidia yoyote kwa ajili ya uhai wa* muuaji anayestahi-

35:22 *Tnn., “bila kumvizia.” 35:30 *Au “anayeu nafsi.” #Au “nafsi itakayouawa.” 35:31 *Au “nafsi ya.”

li kufa, kwa maana ni lazima auawe.^a **32** Nanyi hampaswi kuchukua fidia kwa ajili ya mtu aliyekimbilia katika jiji lake la makimbilio na hivyo kumruhusu arudi kuishi katika ardhi yake kabla ya kuhani mkuu kufa.

33 “Msiichafue nchi mna-yoishi ndani yake, kwa sababu damu inachafua nchi,^b na hakuna msamaha kwa ajili ya damu iliyomwagwa nchini isipokuwa kwa kumwaga damu ya yule aliyeimwaga.^c

34 Msiitie unajisi nchi mna-yoishi ndani yake, ambamo ninakaa; kwa maana mimi, Yehova, ninakaa miongoni mwa Waisraeli.”^d

36 Viongozi wa familia za wazao wa Gileadi mwana wa Makiri^e mwana wa Manase wa koo za wana wa Yosefu wakaja kuzungumza na Musa na wakuu, yaani, viongozi wa makabila ya Waisraeli. **2** Wakawaambia: “Yehova alimwamuru bwana wetu awagawie Waisraeli nchi kwa kura^f ili wairithi; na bwana wetu aliamriwa na Yehova achukue urithi wa Selofehadi ndugu yetu na kuwapa binti zake.^g **3** Lakini wakiolewa na wanaume wa kabila lingine la Waisraeli, urithi wa wanawake hao utaondolewa kutoka katika urithi wa baba zetu na kuongezwa kwenye urithi wa kabila ambamo wataolewa, kwa hiyo urithi huo utaondolewa kutoka katika urithi wetu tuliopokea kwa kura. **4** Waisraeli wanapofanya Mwadhimisho wa Miaka 50,^h urithi wa wanawake hao utaongezwa kwenye urithi wa kabila walimoolewa, na hivyo urithi wao utaondolewa

SURA YA 35

a Mwa 9:5
Kut 21:14
Kum 19:13b Mwa 4:8,10
Zb 106:38
Lu 11:50

c Mwa 9:6

d Kut 25:8
Law 26:12

SURA YA 36

e Hes 26:29

f Hes 26:55
Hes 33:54

g Hes 27:1-7

h Law 25:10

Safu ya 2
a 1Nya 22:22

b Hes 36:6

c Hes 27:1

d Hes 26:3
Hes 33:50
Hes 35:1

kutoka katika urithi wa kabila la baba zetu.”

5 Ndipo Musa akawaamuru hivi Waisraeli kama Yehova alivyoagiza: “Kabila la wana wa Yosefu linasema ukweli.

6 Yehova ameamuru hivi kuhusu mabinti wa Selofehadi: ‘Wanaweza kuolewa na mtu yeyote wampendaye. Lakini wanapaswa kuolewa na mwanamume anayetoka katika ukoo wa kabila la baba yao.

7 Hakuna urithi wa Waisraeli unaopaswa kuhamishwa kutoka kabila moja kwenda kabila lingine, kwa sababu Waisraeli wanapaswa kushikilia urithi wa kabila la mababu zao.

8 Na kila binti aliye na urithi miongoni mwa makabila ya Waisraeli anapaswa kuolewa na mzao wa kabila la baba yake,^a ili Waisraeli waendeleo kumiliki urithi wa mababu zao. **9** Hakuna urithi unaoapaswa kuhamishwa kutoka kabila moja kwenda kabila lingine, kwa sababu makabila ya Waisraeli yanapaswa kushikilia urithi wao.”

10 Mabinti wa Selofehadi walifanya kama Yehova alivyomwamuru Musa.^b **11** Basi Mala, Tirsu, Hogla, Milka, na Noa, mabinti wa Selofehadi,^c waliolewa na wana wa ndugu za baba yao. **12** Wakawa wake za wanaume kutoka katika koo za Manase mwana wa Yosefu, ili urithi wao ubaki katika kabila la baba yao.

13 Hizo ndizo amri na sheria ambazo* Yehova aliwapa Waisraeli kupitia Musa katika jangwa tambarare la Moabu karibu na Yordani, huko Yeriko.^d

36:13 *Tnn., “maamuzi ya hukumu ambayo.”

KUMBUKUMBU LA TORATI

YALIYOMO

- 1 Kuondoka Mlima Horebu (1-8)
Wakuu na waamuzi wawekwa (9-18)
Watu wakosa kutii kule
Kadesh-barnea (19-46)
Waisraeli wakataa kuingia katika ile
nchi (26-33)
Washindwa kuteka Kanaani (41-46)
- 2 Kutangatanga nyikani kwa
miaka 38 (1-23)
Wamshinda Mfalme Sihoni wa
Heshboni (24-37)
- 3 Wamshinda Mfalme Ogu wa
Bashani (1-7)
Kugawanywa kwa nchi upande wa
mashariki wa Yordani (8-20)
Yoshua aambiwa asiogope (21, 22)
Musa hataingia katika nchi hiyo (23-29)
- 4 Waagizwa watii (1-14)
Msisahau matendo ya Mungu (9)
Yehova anataka aabudiwe yeye peke
yake (15-31)
Hakuna Mungu mwingine ila
Yehova (32-40)
Majiji ya makimbilio upande wa
mashariki wa Yordani (41-43)
Wapewa Sheria (44-49)
- 5 Agano la Yehova kule Horebu (1-5)
Amri Kumi zarudiwa (6-22)
Watu waogopa kwenye
Mlima Sinai (23-33)
- 6 Mpende Yehova kwa moyo wako
wote (1-9)
“Sikilizeni, enyi Waisraeli” (4)
Wazazi wanapaswa kuwafundisha
watoto (6, 7)
Msimisahau Yehova (10-15)
Msimjaribu Yehova (16-19)
Kiambiini kizazi kinachofuata (20-25)
- 7 Mataifa saba yataangamizwa (1-6)
Sababu ya Waisraeli kuchaguliwa (7-11)
Utii utawaletea mafanikio wakati
ujao (12-26)
- 8 Baraka kutoka kwa Yehova zatajwa
tena (1-9)
“Haishi kwa mkate tu” (3)
Msimisahau Yehova (10-20)
- 9 Sababu ya Waisraeli kupewa ile
nchi (1-6)
Waisraeli wamkasirisha Yehova mara
nne (7-29)
Ndama wa dhahabu (7-14)
Musa aingilia kati (15-21, 25-29)
Wamkasirisha mara tatu zaidi (22)
- 10 Mabamba mawili yatengenezwa
tena (1-11)
Analotaka Yehova (12-22)
Mwogopeni na kumpenda Yehova (12)
- 11 Mmeuona ukuu wa Yehova (1-7)
Nchi iliyoahidiwa (8-12)
Thawabu za kutii (13-17)
Maneno ya Mungu yakaziwe katika
mioyo (18-25)
“Baraka na laana” (26-32)
- 12 Abuduni mahali ambapo Mungu
amechagua (1-14)
Waruhusiwa kula nyama lakini si
damu (15-28)
Msinaswe na miungu mingine (29-32)
- 13 Jinsi ya kuwatendea waasi imani (1-18)
- 14 Njia zisizofaa za kuomboleza (1, 2)
Vyakula safi na visivyo safi (3-21)
Sehemu ya kumi kwa ajili ya
Yehova (22-29)
- 15 Madeni yafutwa kila mwaka wa
saba (1-6)
Kuwasaidia maskini (7-11)
Kuwaachilia huru watumwa kila
mwaka wa saba (12-18)
Kutoboa sikio la mtumwa kwa
msumari (16, 17)
Wazaliwa wa kwanza wa wanyama
watakaswa (19-23)
- 16 Pasaka; Serehe ya Mikate Isiyo na
Chachu (1-8)
Serehe ya Majuma (9-12)
Serehe ya Vibanda (13-17)
Kuwaweka waamuzi (18-20)
Vitu vya ibada vilivyokatazwa (21, 22)

- 17 Dhabihu zisiwe na kasoro (1)
Kushughulikia uasi imani (2-7)
Kuamua kesi ngumu (8-13)
Maagizo kwa ajili ya mfalme
atakayetawala (14-20)
Mfalme aandike nakala ya Sheria (18)
- 18 Fungu la makuhani na Walawi (1-8)
Mazoea ya kuwasiliana na roho waovu
yakatazwa (9-14)
Nabii kama Musa (15-19)
Jinsi ya kuwatambua manabii wa
uwongo (20-22)
- 19 Hatia ya damu na majiji ya
makimbilio (1-13)
Alama za mipaka zisisogezwe (14)
Mashahidi mahakamani (15-21)
Mashahidi wawili au watatu
wahitajika (15)
- 20 Sheria za vita (1-20)
Wale ambao hawakuruhusiwa
kwenda vitani (5-9)
- 21 Mauaji yaliyofanywa na watu
wasiojulikana (1-9)
Kuoa wanawake mateka (10-14)
Haki ya mzaliwa wa kwanza (15-17)
Mwana mkaidi (18-21)
Mtu aliyetundikwa mtini
amelaaniwa (22, 23)
- 22 Kuheshimu wanyama wa jirani (1-4)
Kuvaa nguo za watu wa jinsia tofauti (5)
Kuwatendea wanyama kwa fadhili (6, 7)
Ukuta unaozunguka ukingo wa paa (8)
Michanganyiko isiyofaa (9-11)
Vishada vya nguo (12)
Sheria kuhusu kukiuka maadili ya
ngono (13-30)
- 23 Wasioruhusiwa katika kutaniko la
Mungu (1-8)
Usafi wa kambi (9-14)
Watumwa waliokimbia (15, 16)
Ukhaba wakatazwa (17, 18)
Riba na nadhiri (19-23)
Vitu ambavyo wapita njia
wanaruhusiwa kula (24, 25)
- 24 Ndoa na talaka (1-5)
Kuheshimu uhai (6-9)
Ku wajali maskini (10-18)
Sheria kuhusu kuokota masalio (19-22)
- 25 Sheria kuhusu kumpiga mtu viboko (1-3)
Usimfunge kinywa ng'ombe dume
anapopura (4)
Ndoa ya ndugu mkwe (5-10)
Kumkamata mtu sehemu zisizofaa
anapopigana (11, 12)
Mizani na vipimo sahihi (13-16)
Waamaleki wataangamizwa (17-19)
- 26 Kutoa mavuno ya kwanza (1-11)
Sehemu ya kumi iliyotolewa mara ya
pili (12-15)
Waisraeli ni mali ya pekee ya
Yehova (16-19)
- 27 Sheria itaandikwa kwenye mawe (1-10)
Kwenye Mlima Ebali na
Mlima Gerizimu (11-14)
Laana zatangazwa (15-26)
- 28 Baraka za kutii (1-14)
Laana za kutotii (15-68)
- 29 Agano pamoja na Waisraeli kule
Moabu (1-13)
Onyo kuhusu kutotii (14-29)
Mambo yaliyofichwa, mambo
yaliyofunuliwa (29)
- 30 Kumrudia Yehova (1-10)
Amri za Yehova si ngumu sana (11-14)
Kuchagua kati ya uzima na kifo (15-20)
- 31 Musa akaribia kufa (1-8)
Sheria yasomwa hadharani (9-13)
Yoshua awekwa kuwa kiongozi (14, 15)
Uasi wa Waisraeli watabiriwa (16-30)
Wimbo wa kuwafundisha
Waisraeli (19, 22, 30)
- 32 Wimbo wa Musa (1-47)
Yehova ni Mwamba (4)
Waisraeli wamsahau Mwamba
wao (18)
"Kisasi ni changu" (35)
"Furahini, enyi mataifa, pamoja na
watu wake" (43)
Musa atafia juu ya Mlima Nebo (48-52)
- 33 Musa ayabariki makabila (1-29)
'Mikono ya milele' ya Yehova (27)
- 34 Yehova amwonyesha Musa ile nchi (1-4)
Kifo cha Musa (5-12)

1 Haya ndiyo maneno ambayo Musa aliwaambia Waisraeli wote walipokuwa nyikani katika eneo la Yordani, katika jangwa tambarare mbele ya Sufi, kati ya Parani, Tofeli, Labani, Haserothi, na Dizahabu. **2** Ni safari ya siku 11 kutoka Horebu mpaka Kadesh-barnea^a kupitia njia ya Mlima Seiri. **3** Katika mwaka wa 40,^b mwezi wa 11, siku ya kwanza ya mwezi huo, Musa aliwaambia Waisraeli* mambo yote ambayo Yehova alimwagiza awaambie. **4** Alifanya hivyo baada ya kumshinda Sihoni^c mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni, na Ogu^d mfalme wa Bashani, aliyekuwa akikaa Ashtarothi, kule Edrei.^e **5** Katika eneo la Yordani nchini Moabu, Musa alianza kuifafanua Sheria^f akisema:

6 "Yehova Mungu wetu alitambua hivi kule Horebu: 'Mmekaa muda wa kutosha katika eneo hili lenye milima.'^g **7** Geukeni na kuelekea katika eneo lenye milima la Waamori^h na kwa majirani wao wote kule Araba,ⁱ katika eneo lenye milima, Shefela, Negebu, pwani ya bahari,^j nchi ya Wakanaani, na Lebanoni,^k hadi kwenye ule mto mkubwa, Mto Efrati.^l **8** Angalieni, nimeweka nchi hii mbele yenu. Ingieni mwililiki nchi ambayo mimi Yehova niliapa kwamba nitawapa baba zenu, Abrahamu, Isaka,^m na Yakobo,ⁿ wao pamoja na uzao wao* baada yao.'^o

9 "Nami niliwaambia ninyi wakati huo, 'Siwezi kuwabeba peke yangu.'^p **10** Ye-

SURA YA 1

- a Kum 9:23
b Hes 32:13
Hes 33:38
c Hes 21:23, 24
Yos 12:1, 2
d Hes 21:33-35
e Yos 13:8, 12
f Kum 4:8
Kum 17:18
Ne 8:7
g Kut 19:1
Hes 10:11, 12
h Mwa 15:16
i Yos 12:2, 3
j Yos 9:1, 2
k Yos 13:1, 5
1Fa 9:19
l Mwa 15:18
m Mwa 26:3
n Mwa 28:13
o Mwa 12:7
Mwa 13:14, 15
Mwa 17:1, 7
p Kut 18:17, 18

Safu ya 2

- a Mwa 15:1, 5
Kut 32:13
Hes 26:51
Kum 10:22
b 1Fa 3:8
c Mwa 12:1-3
Mwa 22:15, 17
Mwa 26:3, 4
Kut 23:25
d Kut 18:17, 18
Hes 11:11
Hes 20:3
e Kut 18:21
f Kut 18:25
g Kut 23:8
Kum 16:18
Yoh 7:24
h Kut 22:21
Law 19:34
Law 24:22
i Law 19:15
Ro 2:11
j Kut 23:3
k Met 29:25
l 2Nya 19:6
m Kut 18:25, 26
n Hes 10:12
Kum 8:14, 15
Yer 2:6
o Hes 13:29

hova Mungu wenu amewafanya mwongezeke, nanyi leo ni wengi kama nyota za mbinguni.^a **11** Yehova Mungu wa mababu zenu na awafanye mwongezeke^b mara elfu moja zaidi ya mlivyo sasa, na awabariki kama alivyowaahidi.^c **12** Mimi peke yangu ninawezaje kuwabeba ninyi ambao ni mzigo pamoja na mizigo yenu na ugomvi wenu?^d **13** Chagueni wanaume wenye hekima, busara, na wenye uzoefu kutoka katika makabila yenu, nami nitawaweka kuwa viongozi wenu.^e **14** Mkanijibu, 'Jambo ulilotuambia ni jema.'^f **15** Basi nikawachukua viongozi wa makabila yenu, wanaume wenye hekima na uzoe fu, na kuwaweka kuwa viongozi wenu, wakuu wa maelfu, wakuu wa mamia, wakuu wa hamsini, wakuu wa makumi, na maofisa wa makabila yenu.^f

16 "Wakati huo niliwaagiza hivi waamuzi wenu: 'Mnaposikiliza kesi kati ya ndugu zenu, mnapaswa kuhukumu kwa uadilifu^g kati ya mtu na ndugu yake au mkaaji mgeni.^h

17 Hampaswi kuhukumu kwa upendeleo.ⁱ Mnapaswa kumsikiliza mdogo kama mnavyomsikiliza mkubwa.^j Msiogopeshwe na wanadamu,^k kwa sababu hukumu ni ya Mungu;^l na ikiwa kesi ni ngumu sana kweni, iletani kwangu, nami nitaisikiliza.'^m **18** Wakati huo nili wapa maagizo kuhusu mambo yote mnapopaswa kufanya.

19 "Kisha tukaondoka Horebu na kupitia ile nyika yote kubwa na yenye kutishaⁿ mliyoona njiani kuelekea kwenye eneo lenye milima la Waamori,^o kama Yehova Mungu wetu alivyotuamuru, na

1:3 *Tnn., "wana wa Israeli." 1:7 *Inaonekana ni safu ya milima ya Lebanoni. 1:8 *Tnn., "mbegu yao."

mwishowe tukafika Kadesh-barnea.^a **20** Halafu nikawaambia, 'Mmfika kwenye eneo lenye milima la Waamori, ambalo Yehova Mungu wetu anatupatia. **21** Angalieni, Yehova Mungu wenu amewapa nchi hii. Pandeni, mkaimiliki, kama Yehova, Mungu wa mababu zenu alivyowaambia.^b Msiogope wala msiwe na hofu.'

22 "Hata hivyo, ninyi nyote mlinijia na kusema, 'Na tume wanaume watutangulie na kuipeleleza nchi kwa ajili yetu, watuletee habari kuhusu njia tunayopaswa kufuata na ni majiji ya aina gani tutakayoyapata huko.'^c **23** Pendekezo hilo lilionekana zuri kwangu, kwa hiyo nikawachagua wanaume 12 miongoni mwa wanaume wenu, mwanamume mmoja kwa ajili ya kila kabila.^d **24** Wakaondoka na kupanda kwenda kwenye eneo lenye milima,^e wakafika kwenye Bonde la Eshkoli na kuipeleleza nchi. **25** Wakachukua baadhi ya matunda ya nchi hiyo na kutuletea, nao wakatuletea habari hii: 'Nchi ambayo Yehova Mungu wetu anatupatia ni nzuri.'^f **26** Lakini mlilikataa kupanda kwenda huko, nanyi mkaliasi agizo la Yehova Mungu wenu.^g **27** Mliendelea kunung'unika katika mahema yenu na kusema, 'Yehova alituchukia ndiyo sababu alitutoa katika nchi ya Misri ili atutie mikononi mwa Waamori watuangamize. **28** Tunaenda mahali pa aina gani? Ndugu zetu walituvunja moyo^h waliposema, "Watu hao wana nguvu zaidi na ni warefu zaidi kuliko sisi,

1:28 *Tnn., "walifanya moyo wetu uye-yuke."

SURA YA 1

a Hes 13:26

b Kut 23:27
Kum 1:8

c Hes 13:1, 2

d Hes 13:3

e Hes 13:17

f Hes 13:23-27

g Hes 14:1-4

h Hes 32:9
Yos 14:7, 8

Safu ya 2

a Hes 13:28, 33

b Hes 13:22
Yos 11:21

c Hes 14:9

d Kut 14:14
Yos 10:42

e Hes 14:22

f Zb 78:22
Zb 106:24
Ebr 3:16, 19
Yud 5g Kut 13:21
Kut 40:36
Hes 10:33, 34
Zb 78:14h Hes 14:28, 35
Hes 32:10-12
Kum 2:14
Zb 95:11
Ebr 3:11i Hes 14:29, 35
1Ko 10:1, 5
Ebr 3:17j Hes 14:24
Yos 14:9k Hes 20:12
Hes 27:13, 14
Kum 3:26
Zb 106:32l Kut 33:11
Hes 11:28

m Hes 14:38

na majiji yao ni makubwa na yana ngome zinazofika mbinguni,^{*a} na huko tuliwaona wana wa Waanaki."^b

29 "Kwa hiyo nikawaambia, 'Msiwe na hofu wala msogope kwa sababu yao.^c **30** Yehova Mungu wenu atawatangulia na kuwapigania,^d kama alivyofanya kule Misri mbele ya macho yenu wenyewe.^e **31** Nanyi miona nyikani jinsi Yehova Mungu wenu alivyowabeba kama baba anavyombeba mwana wake, aliwabeba kila mahali mlipoenda mpaka mlipofika mahali hapa.' **32** Lakini licha ya hayo yote, hamkuwa na imani katika Yehova Mungu wenu,^f **33** aliye kuwa akiwatangulia njiani ili apeleleze mahali mtakapopiga kambi. Alitokea kwa moto wakati wa usiku na kwa wingu wakati wa mchana ili awaonyeshe njia mnayopaswa kufuata.^g

34 "Wakati huo wote Yehova alisikia mambo mliyokuwa mkisema, akakasirika na kuapa hivi:^h **35** 'Hakuna mtu hata mmoja wa kizazi hiki kiovu atakayeona nchi nzuri niliyoapa kwamba nitawapa baba zenu,ⁱ **36** isipokuwa Kalebhu mwana wa Yefune. Yeye ataiona, nami nitampa yeye na wanawe nchi hiyo aliyoikanyaga kwa miguu yake, kwa sababu amenifuata mimi Yehova kwa moyo wote.^{*j} **37** (Yehova alinikasirikia mimi pia kwa sababu yenu, akasema, "Wewe pia hutaingia humo.^k **38** Yohua mwana wa Nuni, mtumishi wako,^{*l} ndiye atakayeingia katika nchi hiyo."^m

1:28 *Yaani, yana kuta ndefu sana. 1:36 *Tnn., "kikamilifu; kabisa." 1:38 *Tnn., "anayesimama mbele yako."

Mwimarishe,^{*a} kwa maana atawawezesha Waisraeli kuirithi nchi hiyo.”) **39** Isitoshe, wato wenu ambao mlisema watakuwa nyara^b na wana wenu ambao leo hawajui lililo jema wala baya, hao ndio watakaolingia katika nchi hiyo, nami nitawapa ili waimiliki.^c **40** Lakini ninyi, geukeni na kwenda nyikani kupitia njia ya Bahari Nyekundu.^d

41 “Ndipo mliponiambia, ‘Tumemtendea Yehova dhambi. Sasa tutapanda kwenda kupigana, kama Yehova Mungu wetu alivyotuumuru!’ Basi kila mmoja wenu akajivika silaha zake za vita, nanyi mlifikiri ni rahisi kupanda mlimani.^e **42** Lakini Yehova akaniambia, ‘Waambie, “Msipande kwenda kupigana, kwa sababu sitakuwa pamoja nanyi.^f Mkienda, maadui wenu watawashinda.”’ **43** Basi nikaongea nanyi, lakini hamkusikiliza. Badala yake, mliasi agizo la Yehova na kujaribu kwa kimbelebele kupanda mlimani. **44** Kisha Waamori waliokuwa wakikaa kwenye mlima huo wakatoka ili kuwashambulia, wakawakimbi za kama nyuki wanavyofanya na kuwatawanya kuanzia Seiri mpaka Horma. **45** Basi mkarudi na kuanza kumlilia Yehova, lakini Yehova hakuwasikiliza wala kuwakazia uangalifu. **46** Ndiyo sababu mliendelea kukaa Kadeshi kwa munda wote mliokaa huko.

2 “Kisha tukageuka na kwenda nyikani kupitia njia ya Bahari Nyekundu, kama Yehova alivyoniambia,^g nasi

1:38 *Au labda, “Mungu amemwimarisha.”

SURA YA 1

a Hes 27:18
Kum 31:7
Yos 1:6, 9

b Hes 14:3

c Hes 14:30, 31

d Hes 14:25

e Hes 14:39-45

f Law 26:14, 17

SURA YA 2

g Hes 14:25

Safu ya 2

a Hes 20:14
Kum 23:7

b Mwa 27:39, 40
Mwa 36:8, 9

c Kut 15:15
Kut 23:27

d Kum 32:8
Yos 24:4
Mdo 17:26

e Hes 20:18, 19

f Kum 29:5
Ne 9:21
Zb 23:1
Zb 34:9, 10

g Hes 20:20, 21

h 2Nya 8:17

i Hes 21:13
Amu 11:17, 18
2Nya 20:10

j Mwa 19:36, 37

k Mwa 14:5

tulizunguka-zunguka Mlima Seiri kwa siku nyingi.

2 Mwishowe Yehova akaniambia hivi: **3** ‘Mmezunguka-zunguka mlima huu kwa muda mrefu vya kutosha. Sasa geukeni mwelekee kaskazini.

4 Nawe uwaamuru watu hivi: “Mtapita karibu na mpaka wa ndugu zenu, wazao wa Esau,^a wanaokaa Seiri,^b nao watawaogopa ninyi,^c basi mnapaswa kuwa waangalifu sana.

5 Msizozane nao,^{*a} kwa sababu sitawapa sehemu yoyote ya nchi yao, hata mahali panapotoshea wayo wa mguu, kwa sababu nimempa Esau Mlima Seiri uwe miliki yake.^d

6 Mnapaswa kuwalipa pesa kwa ajili ya chakula mtaka-chokula, nanyi mnapaswa kulipia maji mtakayokunywa.^e

7 Kwa maana Yehova Mungu wenu amewabariki katika mambo yote mliyofanya. Anajua vizuri kabisa safari yenu katika nyika hii kubwa. Yehova Mungu wenu amekuwa pamoja nanyi kwa miaka hii 40, nanyi hamjakosa kitu chochote.”^f **8** Basi tuliwapa ndugu zetu, wazao wa Esau,^g wanaokaa Seiri, tukaepuka njia ya Araba, kutoka Elathi na kutoka Esion-geberi.^h

“Kisha tukageuka na kupitia njia ya nyika ya Moabu.ⁱ **9** Ndipo Yehova akaniambia, ‘Msizozane wala kupigana na Wamoabu, kwa sababu sitawapa ninyi sehemu yoyote ya nchi yao ili mwimiliki kwa sababu nimewapa wazao wa Loti^j nchi ya Ari ili waimiliki. **10** (Waemi^k waliishi katika nchi hiyo zamani, walikuwa watu wenye nguvu na

2:5 *Au “Msiwachokeze.”

wengi sana na warefu kama Waanaki. **11** Warefaimu^a pia walionwa kama Waanaki,^b na Wamoabu walikuwa wakiwaita Waemi. **12** Awali, Wahori^c waliishi Seiri, lakini wazao wa Esau walimiliki nchi yao, wakawaangamiza na kukaa humo badala yao,^d kama Waisraeli watakvayofanya katika nchi ambayo ni miliki yao, ambayo kwa hakika Yehova atawapa.) **13** Sasa nendeni mvuke Bonde* la Zeredi.' Basi tukavuka Bonde la Zeredi.^e **14** Tulitembea kwa miaka 38 kutoka Kadesh-barnea mpaka tulipovuka Bonde la Zeredi, mpaka kizazi chote cha wanaume wa vita kilipoangamia kutoka kambini, kama Yehova alivyokuwa amewaapia.^f **15** Mkono wa Yehova uliwapinga ili kuwaangamiza kutoka kambini mpaka walipoisha.^g **16** "Mara tu wanaume wote wa vita walipokufa,^h **17** Yehova akazungumza nami tena, akaniambia, **18** 'Leo mtapita karibu na eneo la Moabu, yaani, Ari. **19** Mtakapofika karibu na Waamoni, msiwachokoze wala kuzozana nao, kwa sababu sitawapa ninyi nchi yoyote ya Waamoni ili mwimiliki, kwa kuwa nimewapa wazao wa Loti waimiliki.ⁱ **20** Nchi hiyo pia ilionwa kuwa nchi ya Warefaimu.^j (Warefaimu waliishi katika nchi hiyo zamani, na Waamoni walikuwa wakiwaita Wazamuzmi. **21** Walikuwa watu wenye nguvu na wengi sana na warefu kama Waanaki;^k lakini Yehova aliwasaidia Waamoni kuwaangamiza, Waamoni wakawafukuza na kuishi humo ba-

2:13, 24 *Au "Korongo."

SURA YA 2

a Kum 3:11
1Nya 20:6

b Hes 13:22, 33

c Mwa 14:6
Mwa 36:20

d Mwa 27:39, 40

e Hes 21:12

f Hes 14:33
Hes 32:11
Kum 1:35
Zb 95:11
Ebr 3:18
Yud 5

g 1Ko 10:1, 5

h Hes 26:63, 64

i Mwa 19:36, 38
Kum 2:9
Amu 11:15
2Nya 20:10
Mdo 17:26

j Mwa 15:18-20
Kum 3:11

k Hes 13:33
Kum 9:1, 2

Safu ya 2

a Mwa 36:8

b Mwa 14:6
Kum 2:12

c Mwa 10:19

d Mwa 10:13, 14

e Hes 21:13

f Hes 21:23

g Kut 15:14
Kut 23:27
Kum 11:25
Yos 2:9, 10

h Yos 13:15, 18
Yos 21:8, 37

i Kum 20:10

j Hes 11:21, 22

dala yao. **22** Hivyo ndivyo alivyofanya kwa ajili ya wazao wa Esau, ambao sasa wanakaa Seiri,^a alipowaangamiza Wahori^b kutoka mbele yao, ili wamiliki nchi yao na kukaa humo badala yao mpaka leo. **23** Nao Waavi, walikuwa wakiishi katika vijiji vilivyofika Gaza,^c mpaka Wakaftori waliotoka Kaftori*^d walipokuja na kuwaangamiza na kukaa humo badala yao.)

24 "Ondokeni, mvuke Bonde* la Arnoni.^e Tazameni nimemtia mikononi mwenu Sihoni^f Mwamori, mfalme wa Heshboni. Basi anzeni kumiliki nchi yake, nanyi mpigane vita naye. **25** Siku ya leo nitaanza kuwafanya watu wote duniani* wanaosikia habari zenu wawahofu na kuwaogopa ninyi. Watakuwa na wasiwasi na kutetemeka^g kwa sababu yenu."^g

26 "Kisha kutoka katika nyika ya Kedemothi,^h niliwa-tuma wajumbe kwa Mfalme Sihoni wa Heshboni, ili wampe ujumbe huu wa amani:ⁱ **27** 'Niruhusu nipite katika nchi yako. Nitatembea barabarani tu, sitakwenda kulia wala kushoto.^j **28** Nitakula tu chakula na kunywa tu maji utakayoniuzia. Niruhusu tu nipite kwa miguu, **29** hivyo ndivyo wazao wa Esau wanaokaa Seiri na Wamoabu wanaokaa Ari walivyoni-fanyia, mpaka nitakapovuka Yordani na kuingia nchi ambayo Yehova Mungu wetu anata-pa sisi.' **30** Lakini Mfalme Sihoni wa Heshboni

2:23 *Yaani, Krete. 2:25 *Tnn., "walio chini ya mbingu." ^g Au "watakuwa na uchungu kama wa kuzaa."

hakaturuhusu tupite, kwa sababu Yehova Mungu wenu alimwacha awe na roho ya ukaidi^a na moyo wake uwe mguumu, ili amtie mikononi mwenu kama ilivyo leo.^b

31 “Kisha Yehova akaniaambia, ‘Angalieni, tayari nimeanza kumtia mikononi mwenu Sihoni pamoja na nchi yake. Anzeni kuimiliki nchi yake.’^c

32 Sihoni alipotoka na watu wake wote ili kupigana nasi kule Yahazi,^d **33** Yehova Mungu wetu alimtia mikononi mwetu, hivi kwamba tukamshinda yeye, wanawe, na watu wake wote. **34** Tuliteka majiji yake yote wakati huo na kuangamiza kila jiji, pamoja na wanaume, wanawake, na watoto. Hatukumwacha mtu yeyote akiwa hai.^e **35** Tulijichukulia tu mifugo pamoja na nyara za majiji tuliyokuwa tumeteka. **36** Kuanzia Aroeri,^f jiji lililo kwenye ukingo wa Bonde* la Arnoni (pamoja na jiji lililo bondeni), mpaka Gileadi, hakuna mji wowote ambao hatungeweza kuuteka. Yehova Mungu wetu aliitia yote mikononi mwetu.^g **37** Hata hivyo, hamkukaribia nchi ya Waamoni,^h ukingo wote wa Bonde* la Yabokiⁱ na majiji yaliyo kwenye eneo lenye milima, wala eneo lingine lolote tulilokatizwa na Yehova Mungu wetu.

3 “Kisha tuligeuka na kupanda kupitia Njia ya Bashani. Ndipo Ogu, mfalme wa Bashani, akatoka pamoja na watu wake wote ili kupigana vita nasi kule Edrei.^j

2:36, 37; 3:8 *Au “Korongo.”

SURA YA 2

a Ro 9:18

b Hes 21:25

c Hes 32:33
Zb 135:10-12d Hes 21:23, 24
Amu 11:20

e Kum 20:16, 17

f Kum 3:12
Kum 4:47, 48
Yos 13:8, 9

g Zb 44:3

h Kum 3:16
Amu 11:15

i Hes 21:23, 24

SURA YA 3

j Hes 21:33-35

Safu ya 2

a Hes 32:33
Kum 29:7, 8
Yos 13:29, 30

b Law 27:29

c Law 18:25

d Hes 32:33

e Yos 12:1, 2

f Hes 21:33

2 Basi Yehova akaniaambia, ‘Usimwogope, kwa maana nitamtia mikononi mwako pamoja na watu wake wote na nchi yake, nawe utamtendea kama ulivyomtendea Sihoni mfalme wa Waamori, aliyeshi Heshboni.’ **3** Basi Yehova Mungu wetu akamtia pia mikononi mwetu Mfalme Ogu wa Bashani pamoja na watu wake wote, nasi tukaendelea kumshambulia hivi kwamba hakuna mtu yeyote kati ya watu wake aliyekoka. **4** Kisha tukateka majiji yake yote. Hakuna mji wao hata mmoja ambao hatukuuteka, tuliteka majiji 60 katika eneo lote la Argobu, yaani, ufalme wa Ogu kule Bashani.^a **5** Majiji hayo yote yalikuwa na kuta ndefu zenye ngome, malango, na makomeo, tuliteka pia miji mingi sana ya mashambani. **6** Hata hivyo, tuliwaangamiza,^b kama tulivyomwangamiza Mfalme Sihoni wa Heshboni, tuliangamiza kila jiji, kutia ndani wanaume, wanawake, na watoto.^c **7** Nasi tukajichukulia mifugo yote na nyara za majiji hayo.

8 “Wakati huo tulichukua nchi ya wafalme wawili wa Waamori^d waliokuwa katika eneo la Yordani, kuanzia Bonde* la Arnoni mpaka Mlima Hermoni^e **9** (Wasidoni waliokuwa wakiuita mlima huo Sirioni, nao Waamori walikuwa wakiuita Seniri), **10** majiji yote yaliyokuwa katika nchi tambarare, nchi yote ya Gileadi, nchi yote ya Bashani mpaka Saleka na Edrei,^f majiji ya ufalme wa Ogu kule Bashani. **11** Kwa maana Mfalme Ogu wa Bashani ndiye Mrefaimu pekee aliyekuwa amebaki. Jeneza lake lilitengenezwa

kwa chuma,* na bado liko katika jiji la Waamoni la Raba. Lina urefu wa mikono tisa[#] na upana wa mikono minne, kulingana na kipimo cha kawaida cha mkono. **12** Wakati huo tulimiliki nchi hii: kuanzia Aroeri,^a karibu na Bonde* la Arnoni, na nusu ya eneo lenye milima la Gileadi, na majiji yake nimewapa watu wa kabila la Rubeni na kabila la Gadi.^b **13** Kisha nusu ya kabila la Manase^c nimewapa sehemu inayobaki ya Gileadi na eneo lote la Bashani la ufalme wa Ogu. Eneo lote la Argobu, la Bashani, lilijulikana kuwa nchi ya Warefaimu.

14 "Yairi^d mwana wa Manase alichukua eneo lote la Argobu^e hadi kwenye mpaka wa Wageshuri na Wamaakathi,^f akaviita vijiji hivyo vya Bashani kwa jina lake mwenyewe, Hawoth-yairi,^g mpaka leo. **15** Naye Makiri nimempa Gileadi.^h **16** Na watu wa kabila la Rubeni na kabila la Gadiⁱ nimewapa kuanzia Gileadi mpaka kwenye Bonde* la Arnoni, katikati ya bonde ulikuwa ndio mpaka, hadi Bonde la Yaboki, ambalo ni mpaka wa Waamoni, **17** na Araba na Yordani na ule mpaka, kuanzia Kinereithi hadi Bahari ya Araba, Bahari ya Chumvi, chini ya mteremko wa Pisga chuelekea upande wa mashariki.^j

18 "Kisha nikawaamuru hivi: 'Yehova Mungu wenu amewapa nchi hii mwimiliki. Wanaume wenu wote mashu-

3:11 *Au "jiwe jeusi la volkano." #Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. 3:12, 16 *Au "Korongo." 3:14 *Maana yake "Vijiji vya Mahema vya Yairi."

SURA YA 3

a Hes 32:34

b Hes 32:33

c Hes 32:39
Yos 13:29-31
1Nya 5:23

d 1Nya 2:22

e Kum 3:4

f Yos 13:13

g Hes 32:40, 41

h Hes 32:39
Yos 17:1i Hes 32:33
Yos 22:9

j Hes 34:11, 12

Safu ya 2

a Hes 32:20-22

b Yos 1:14, 15
Yos 22:4, 8c Hes 11:28
Hes 14:30
Hes 27:18

d Yos 10:25

e Kut 14:14
Kut 15:3
Kum 1:30
Kum 20:4
Yos 10:42f Kut 15:16
Kum 11:2g Kut 15:11
2Sa 7:22
1Fa 8:23
Zb 86:8
Yer 10:6, 7h Kut 3:8
Kum 1:7
Kum 11:11, 12i Hes 20:12
Hes 27:13, 14
Kum 4:21
Zb 106:32

jaa watachukua silaha na kuvuka mbele ya ndugu zenu, Waisraeli.^a **19** Lakini wake zenu, watoto wenu, na wanyama wenu tu (najua vizuri kwamba mna wanyama wengi sana) ndio watakoendelea kukaa katika majiji ambayo nimewapa, **20** mpaka Yehova atakapowapumzisha ndugu zenu, kama anavyowapumzisha ninyi, nao pia waimiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa ng'ambo ya Yordani. Ndipo mtakaporudi, kila mmoja atarudi kwenye miliki yake ambayo nimempa.^b

21 "Wakati huo nilimwamuru hivi Yoshua:^c 'Umeona kwa macho yako mwenyewe mambo ambayo Yehova Mungu wako amewatendea wafalme hao wawili. Hivyo ndivyo Yehova atakavyozitendea falme zote huko mnakovuka kwenda.^d **22** Msiwaogope, kwa maana Yehova Mungu wenu ndiye anayewapigania ninyi.^e

23 "Wakati huo nilimsihi hivi Yehova: **24** 'Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, umeanza kumwonyesha mtumishi wako ukuu wako na mkono wako wenye nguvu,^f kwa maana ni mungu gani mbinguni au duniani anayetenda mambo makuu kama wewe?^g **25** Tafadhali niruhusu nivuke na kuona nchi nzuri iliyo ng'ambo ya Yordani, eneo hili zuri lenye milima na Lebanoni.^h **26** Lakini bado Yehova alikuwa amenikasirikia vikali kwa sababu yenu,ⁱ naye hakutaka kunisikiliza. Badala yake Yehova ali-niambia, 'Imetosha! Usizungumze nami tena kamwe kuhusu

jambo hili. **27** Panda juu ya kilele cha Pisga,^a utazame magharibi na kaskazini na kusini na mashariki, uone nchi hiyo kwa macho yako, kwa maa-na hutavuka mto huu wa Yordani.^b **28** Nawe umweke Yohshua^c kuwa kiongozi, umtie moyo na kumwimarisha, kwa sababu yeye ndiye atakaye-waongoza watu hawa kuvuka^d na kuwawezesha kuirithi nchi utakayoiona.' **29** Mambo hayo yote yalitendeka tulipokuwa tukikaa katika bonde lililo mbele ya Beth-peori.^e

4 "Sasa, enyi Waisraeli, siki-lizeni masharti na sheria ambazo* ninawafundisha kushika, ili mwishif na kuingia kuimiliki nchi ambayo Yehova, Mungu wa mababu zenu, anawapa ninyi. **2** Hampaswi kuongeza jambo lolote kwenye neno ninalowaamuru, wala kuondoa jambo lolote kutoka katika neno hilo,^g ili mzi-shike amri za Yehova Mungu wenu ninazowaamuru ninyi.

3 "Macho yenu wenyewe yameona mambo ambayo Yehova alitenda kuhusiana na kisa cha Baali wa Peori; Yehova Mungu wenu alimwangamiza kila mtu miongoni mwenu aliyemfuata Baali wa Peori.^h **4** Lakini ninyi mnaoshikamana kabisa na Yehova Mungu wenu, nyote mko hai leo. **5** Tazameni, nimewafundisha masharti na sheria,* kama nilivyoamriwa na Yehova Mungu wangu, ili mzi-shike katika nchi mtakayomiliki. **6** Ni lazima mzifuate kwa uangalifu,^j kwa sababu watu watakaosikia kuhusu masharti haya

4:1 *Tnn., "maamuzi ya hukumu ambayo." 4:5, 8 *Tnn., "maamuzi ya hukumu."

SURA YA 3

- a Hes 27:12
b Kum 34:1, 4
c Hes 27:18-20
Kum 1:38
Kum 31:7
d Yos 1:1, 2
e Kum 4:45, 46
Kum 34:5, 6

SURA YA 4

- f Law 18:5
g Kum 12:32
Met 30:5, 6
Ufu 22:18, 19
h Hes 25:5, 9
Zb 106:28
Ho 9:10
1Ko 10:7, 8
i Law 26:46
Hes 30:16
Hes 36:13
Kum 6:1
j 1Fa 2:3

Safu ya 2

- a Zb 111:10
b Zb 119:98, 100
c 1Fa 4:34
1Fa 10:4-7
Da 1:19, 20
d Kut 25:8
Law 26:12
Kum 5:26
2Sa 7:23
e Zb 147:19, 20
f Mwa 18:19
Kum 6:6, 7
g Kut 19:9
h Kut 20:20
Kum 5:29
i Met 22:6
Efe 6:4
j Kut 19:18
Ebr 12:18, 19
k Kum 9:10
l Isa 40:18
Yoh 1:18
Yoh 4:24
m Kut 20:22
n Kut 19:5
Kum 5:2
Kum 9:9
Ebr 9:19, 20
o Kut 20:1
Kut 34:28
Kum 10:4
p Kut 24:12
Kut 31:18
Kut 32:19
Kut 34:1

yote wataona kwamba mna hekima^a na uelewaji,^b nao watasema, 'Kwa hakika watu wa taifa hili kubwa wana hekima na uelewaji.'^c **7** Kwa maa-na ni taifa gani kubwa ambalo miungu yake iko karibu nalo kama Yehova Mungu wetu alivyo karibu nasi wakati wowote tunapomlilia?^d **8** Na ni taifa gani kubwa ambalo lina masharti ya uadilifu na sheria* kama Sheria hii yote ninayowe-ka mbele yenu leo?^e

9 "Ila tu muwe waangalifu na kujihadhari sana, ili msisahau mambo ambayo macho yenu yameona na ili yasiondo-ke moyoni mwenu siku zote za maisha yenu. Ni lazima pia muwaambie wana wenu na wajukuu wenu.^f **10** Siku ambayo mlisimama mbele za Yehova Mungu wenu kule Horebu, Yehova aliniambia, 'Wakusanye watu mbele zangu ili niwafanye wasikie maneno yangu,^g ili wajifunze kuniogopa^h siku zote ambazo watakuwa hai juu ya ardhi na ili wawafundishe wana wao.'ⁱ

11 "Basi mlifikaribia na kusimama chini ya mlima, na mlima huo ulikuwa ukiwaka moto uliofika mpaka mbinguni; kulikuwa na giza, wingu, na utusitusi mzito.^j **12** Yehova akaanza kuzungumza nanyi kutoka katika moto.^k Mlisikia maneno, lakini hamkuona umbo lolote^l—kulikuwa na sauti tu.^m **13** Naye akawatangazia agano lake,ⁿ alilowaamuru mshike—zile Amri Kumi.^{*o} Kisha akaziandika kwenye mabamba mawili ya mawe.^p **14** Wakati huo, Yehova aliniamuru niwafundishe masharti na sheria amba-

4:13 *Tnn., "yale Maneno Kumi."

zo* mnapaswa kushika katika nchi mtakayoingia kuimiliki.

15 “Kwa hiyo, jihadharini sana—kwa sababu hamkuona umbo lolote siku ambayo Yehova alizungumza nanyi kule Horebu kutoka katikati ya moto— **16** ili msitende upotovu kwa kujitengezea sanamu ya kuchongwa yenye umbo la mfano wowote, mfano wa mwanamume au mwanamke,^a **17** mfano wa mnyama yeyote duniani au mfano wa ndege yeyote anayeruka angani,^b **18** mfano wa kitu chochote kinachotambaa ardhini au mfano wa samaki yeyote aliye ndani ya maji chini ya dunia.^c **19** Nanyi mnapoinua macho yenu kutazama mbinguni na kuona jua na mwezi na nyota—jeshi lote la mbinguni—msishawishiwe kuviinamia na kuvia-budu.^d Yehova Mungu wenu amewapa watu wote duniani* vitu hivyo. **20** Lakini ninyi ndio watu ambao Yehova aliwatoa katika tanuru la kuyeyushia chuma, kutoka Misri, ili muwe watu ambao ni mali yake*^e mwenyewe, kama mliyoyo leo.

21 “Yehova alinikasirikia kwa sababu yenu,^f akaapa kwamba sipaswi kuvuka Yordani au kuingia katika nchi nzuri ambayo Yehova Mungu wenu anawapa iwe urithi wenu.^g **22** Kwa maana nitakufa katika nchi hii; sitavuka Yordani,^h lakini ninyi mtavuka na kuimiliki nchi hiyo nzuri. **23** Iweni waangalifu msisahau agano la Yehova Mungu wenu ambalo alifanya pamo-

4:14 *Tnn., “maamuzi ya hukumu ambayo.” 4:19 *Tnn., “walio chini ya mbingu.” 4:20 *Au “urithi wake.”

SURA YA 4

a Kut 20:4
Kum 27:15
Isa 40:18
Mdo 17:29
1Ko 10:14

b Kum 5:8
Ro 1:22, 23

c 1Sa 5:4

d Kum 17:2, 3
2Fa 17:16
Eze 8:16

e Kut 19:5

f Zb 106:32

g Hes 20:12
Kum 31:1, 2

h Kum 3:27

Safu ya 2

a Kut 24:3

b Kut 20:4

c Kut 24:17
Kum 9:3
Ebr 12:29

d Kut 20:5
Kut 34:14
Hes 25:11
Lu 10:27

e Amu 18:30
2Fa 21:1, 7

f 2Fa 17:16, 17

g Law 18:24, 28
Law 26:27, 32

h Kum 28:64
Ne 1:8

i Kum 28:62

j Kum 28:15, 36
Yer 16:13
Eze 20:39

k 2Nya 15:4, 15

l Kum 30:1-3
Kum 30:8-10
1Fa 8:48, 49
Yer 29:13
Yoe 2:12

ja nanyi,^a na msijitengezee sanamu ya kuchongwa, umbo la kitu chochote mlichokatazwa na Yehova Mungu wenu.^b

24 Kwa maana Yehova Mungu wenu ni moto unaoteketeza,^c Mungu anayetaka watu wamwabudu yeye peke yake.^d

25 “Ikiwa mtazaa wana na wajukuu na kuishi kwa muda mrefu nchini nanyi mtende upotovu na kutengezea sanamu ya kuchongwa^e ya aina yoyote na kutenda uovu machoni pa Yehova Mungu wenu na hivyo kumkasirisha,^f **26** nachukua mbingu na dunia ili ziwe mashahidi dhidi yenu leo ya kwamba kwa haki-ka mtaangamia haraka kutoka katika nchi mnapovuka Yordani kwenda kuimiliki. Hamtashi kwa muda mrefu katika nchi hiyo, badala yake mtaangamizwa kabisa.^g **27** Yehova atawatawanya miongoni mwa mataifa,^h na ni watu wachache tu kati yenu watakaokokaⁱ miongoni mwa mataifa ambayo Yehova atawafukuza ninyi mwende miongoni mwa. **28** Huko mtalazimika kuiabudu miungu ya miti na mawe iliyotengenezwa kwa mikono ya wanadamu,^j miungu ambayo haiwezi kuona wala kusikia wala kula wala kunusa.

29 “Mkimtafuta Yehova Mungu wenu mkiwa huko, haki-ka mtampata,^k naam, mkiutafuta ushauri wake kwa moyo wenu wote na kwa nafsi* yenu yote.^l **30** Baa-daye mtakapokuwa mkiteseka sana na mambo hayo yote yatakapokuwa yamewapata, ndipo mtakapomrudia Yehova

4:29 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

Mungu wenu na kuisikiliza sauti yake.^a **31** Kwa maana Yehova Mungu wenu ni Mungu mwenye rehema.^b Hatawaacha wala kuwaangamiza wala kusahau agano alilowaa-pia mababu zenu.^c

32 “Sasa, ulizeni kuhusu siku za zamani kabla ya ninyi kuwepo, tangu siku ambayo Mungu alimuumba mwana-damu duniani; tafuteni kuanzia mwisho mmoja wa mbingu mpaka mwisho mwingine wa mbingu. Je, kuna jambo lolote kubwa kama hili ambalo limewahi kutokea au kuna jambo lolote kama hili ambalo limewahi kusikiwa?^d **33** Je, kuna taifa lingine lolote ambalo limewahi kusikia sauti ya Mungu ikisema kutoka katika moto kama ninyi mlivyosikia na kuendelea kuishi?^e

34 Au je, Mungu amewahi kujaribu kujichukulia taifa kutoka kati ya taifa lingine kwa hukumu,* kwa ishara, kwa miujiza,^f kwa vita,^g kwa mkono wenye nguvu,^h kwa mkono ulionyoshwa, na kwa mateendo ya kutisha,ⁱ kama Yehova Mungu wenu alivyowafanyia kule Misri mbele ya macho yenu wenyewe? **35** Ninyi wenyewe mmeonyeshwa mambo hayo ili mjue kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli; haku-na mwingine isipokuwa yeye.^k **36** Aliwawezesha kusikia sauti yake kutoka mbinguni ili awarekebishe, na duniani aliwawezesha kuona moto wake mkubwa, na maneno yake mliyasia kutoka katika moto.^l

37 “Kwa sababu aliwape-nda mababu zenu na amechagua uzao wao* baada yao,^m

4:34 *Au “majaribu.” 4:37 *Tnn., “mbegu yao.”

SURA YA 4

a 2Nya 33:13
Ne 1:9

b Kut 34:6
Kum 30:3
2Nya 30:9
Ne 9:31
Isa 54:7
Isa 55:7

c Law 26:42

d Zb 44:1

e Kum 5:26

f Kut 7:3

g Kut 15:3

h Kut 13:3

i Kum 26:8
Zb 78:43-51

j Kut 6:7

k Kut 15:11
Kum 32:39
1Sa 2:2
Isa 45:18
Mk 12:32

l Kut 19:18
Kut 20:22

m Kum 10:15
Zb 105:6

Safu ya 2

a Kut 23:28
Kum 7:1
Kum 9:1
Yos 3:10

b 2Nya 20:6

c Isa 44:6

d Mwa 48:3, 4

e Hes 35:14

f Hes 35:22-24

g Hes 35:11, 25
Kum 19:4, 5

h Yos 21:8, 36

i Yos 21:8, 38

j Yos 21:27

k Yos 20:8, 9

l Kum 17:18
Kum 27:2, 3
Gal 3:24

m Law 26:46
Kum 4:1

n Kum 1:5
Kum 3:29

naye aliwatoa Misri kwa nguvu zake kuu mbele ya macho yake. **38** Naye aliyafukuza kutoka mbele yenu mataifa makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko ninyi, ili awa-lete ninyi katika nchi yao na kuwapa iwe urithi wenu, kama ilivyo leo.^a **39** Kwa hiyo, siku ya leo, mjue na kutia moyoni kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli juu mbinguni na chini duniani.^b Hakuna mwingine.^c **40** Ni lazima mshike masharti yake na amri zake ni-nazowapa ninyi leo, ili mambo yawaendee vyema ninyi na wana wenu baada yenu, ili mwendelee kuishi kwa muda mrefu katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa.”^d

41 Wakati huo Musa alitenga majiji matatu upande wa mashariki wa Yordani.^e **42** Mtu yeyote anayemua mwenzake bila kukusudia na hakuwa akimchukia,^f ni lazima akimbilie katika mojawapo ya majiji hayo ili aishi.^g **43** Majiji hayo ni Beseri^h kule nyikani katika uwanda wa juu kwa ajili ya watu wa kabila la Rubeni, Ramothiⁱ kule Gileadi kwa ajili ya watu wa kabila la Gadi, na Golani^j kule Bashani kwa ajili ya watu wa kabila la Manase.^k

44 Basi hiyo ndiyo Sheria^l ambayo Musa aliwapa Waisraeli. **45** Hivyo ndivyo vikumbusho, masharti, na sheria ambazo* Musa aliwapa Waisraeli baada ya kutoka Misri,^m **46** katika eneo la Yordani, kwenye bonde lililo ng'ambo ya Beth-peori,ⁿ katika nchi ya Mfalme Sihoni wa

4:45 *Tnn., “maamuzi ya hukumu ambayo.”

Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni,^a ambaye Musa na Waisraeli walimshinda walipotoka Misri.^b **47** Nao wakaimiliki nchi yake na nchi ya Mfalme Ogu^c wa Bashani, wafalme wawili wa Waamori walio-kuwa katika eneo lililokuwa upande wa mashariki wa Yordani, **48** kuanzia Aroeri,^d kwenye ukingo wa Bonde la Arnoni, mpaka Mlima Sioni, yaani, Hermoni,^e **49** na eneo lote la Araba upande wa mashariki wa Yordani, mpaka Bahari ya Araba,^{*} chini ya mitememko ya Pisga.^f

5 Kisha Musa akawaita Waisraeli wote na kuwaambia hivi: “Enyi Waisraeli, sikilizeni masharti na sheria ambazo* ninawatangazia ninyi leo, nanyi mnapaswa kujifunza na kushika kwa uangalifu masharti na sheria hizo. **2** Yehova Mungu wetu alifanya agano pamoja nasi kule Horebu.^g **3** Yehova hakufanya agano hilo pamoja na mababu zetu, bali pamoja nasi, sisi sote tulio hai hapa leo. **4** Yehova alizungumza nanyi uso kwa uso mlimani, kutoka katika moto.^h **5** Wakati huo nilisimama kati yenu na Yehova ili niwaambie neno la Yehova, kwa maana mliogopa kwa sababu ya moto nanyi hamkupa-nda mlimani.ⁱ Alisema hivi:

6 “Mimi ni Yehova Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa.^k **7** Hupaswi kamwe kuwa na miungu mingine ila mimi.^{*j}

4:49 *Yaani, Bahari ya Chumvi. **5:1** *Tnn., “maamuzi ya hukumu ambayo.” **5:7** *Au “dhidi yangu.” Tnn., “dhidi ya uso wangu.”

SURA YA 4

a Hes 21:26

b Hes 21:23, 24

c Hes 21:33
Kum 3:4d Kum 2:36
Kum 3:12

e Kum 3:8, 9

f Kum 3:16, 17
Kum 34:1

SURA YA 5

g Kut 19:5
Ebr 9:19, 20h Kut 19:9, 18
Mdo 7:38i Kut 20:19
Gal 3:19

j Kut 19:16

k Kut 13:3
Kut 20:2l Kut 20:3-6
2Fa 17:35

Safu ya 2

a Law 26:1
Kum 4:15, 16
Kum 4:23
Kum 27:15
Mdo 17:29b Kut 23:24
1Ko 10:14c Kut 34:14
Kum 4:24
Isa 42:8
Mt 4:10

d Kut 34:6, 7

e Kut 22:28
Law 19:12f Kut 20:7
Law 24:16g Kut 16:23
Kut 20:8-10
Kut 31:13

h Kut 34:21

i Kut 16:29

j Ne 13:15

k Kut 23:12

l Kum 10:17
Efe 6:9

8 “Usijitengenezee sanamu ya kuchongwa^a au mfano wa* kitu chochote kilicho juu mbinguni au kilicho chini duniani au kilicho ndani ya maji chini ya dunia. **9** Usiviamie wala kushawishiwa kuviabudu,^b kwa sababu mimi, Yehova Mungu wako, ni Mungu ninayetaka watu waniabudu mimi peke yangu,^c nami huwaadhibu watoto kwa sababu ya makosa ya baba zao, kufikia kizazi cha tatu na kizazi cha nne cha wale wanaonichukia,^d **10** lakini ninawatendea kwa upendo mshikamanifu* watu wanaonipenda na kushika amri zangu, kufikia kizazi chao cha elfu.

11 “Usilitumie jina langu mimi, Yehova Mungu wako, kwa njia isiyofaa,^e kwa maana mimi Yehova sitakosa kumwadhibu yule anayetumia jina langu kwa njia isiyofaa.^f

12 “Ishike siku ya Sabato na uione kuwa takatifu, kama mimi Yehova Mungu wako nilivyokuamuru.^g **13** Fanya shughuli na kazi zako zote kwa siku sita,^h **14** lakini siku ya saba ni sabato kwa Yehova Mungu wako.ⁱ Usifanye kazi yoyote,^j wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala kijakazi wako, wala ng'ombe dume wako, wala punda wako, wala mnyama yeyote unayemfuga, wala mgeni anayekaa katika majiji*^k yenu, ili mtumwa wako na kijakazi wako wapumzike kama wewe.^l **15** Kumbuka kwamba ulikuwa mtumwa nchini Misri, na mimi Yehova Mungu wako nikakutoa

5:8 *Au “umbo la.” **5:10** *Au “fadhili zenye upendo.” **5:14** *Tnn., “malango.”

huko kwa mkono wenye nguvu na mkono ulionyoochwaa.^a Ndiyo sababu mimi Yehova Mungu wako nilikuamuru uishike siku ya Sabato.

16 “Mheshimu baba yako na mama yako,^b kama mimi Yehova Mungu wako nilivyo-kuamuru, ili uishi muda mrefu na kufanikiwa* katika nchi ambayo mimi Yehova Mungu wako ninakwa.^c

17 “Usiue.^d

18 “Wala usifanye uzinzi.^e

19 “Wala usiibe.^f

20 “Wala usitoe ushahidi wa uwongo dhidi ya jirani yako.^g

21 “Wala usimtamani mke wa jirani yako.^h Wala usitamani kwa ubinafsi nyumba ya jirani yako, wala shamba lake, wala mtumwa wake, wala kijakazi wake, wala ng’ombe dume wake, wala punda wake, wala kitu chochote cha jirani yako.ⁱ

22 “Yehova aliwapa amri hizo* ninyi nyote mlimani, kutoka katika moto, wingu, na utusitusi mzito,^j kwa sauti kubwa, naye hakuongeza lolote; kisha akaziandika kwenye mabamba mawili ya mawe na kunipa.^k

23 “Lakini mara tu mliposikia sauti kutoka katika lile giza, mlima ulipokuwa ukiwaka moto,^l viongozi wote wa makabila yenu na wazee wakanijia. **24** Kisha mkasema, ‘Tazama, Yehova Mungu wetu ametuonyesha utukufu wake na ukuu wake, nasi tumesikia sauti yake kutoka katika moto.^m Leo tumeona kwa mba Mungu anaweza kuongea

5:16 *Au “na ili mambo yakuendee vyema.” 5:22 *Tnn., “maneno hayo.”

SURA YA 5

- a Kut 6:6
Kum 4:34
- b Kut 21:15
Law 19:3
Kum 27:16
Met 1:8
Mk 7:10
- c Kut 20:12
Efe 6:2, 3
- d Mwa 9:6
Kut 20:13
Hes 35:20, 21
Mt 5:21
Ro 13:9
- e Kut 20:14
1Ko 6:18
Efe 6:2
- f Kut 20:15
Law 19:11
Met 30:8, 9
1Ko 6:10
Efe 4:28
- g Kut 20:16
Kut 23:1
Law 19:16
Kum 19:16-19
Met 6:16, 19
Met 19:5
- h Mt 5:28
- i Kut 20:17
Lu 12:15
Ro 7:7
- j Kut 19:9, 18
- k Kut 24:12
Kut 31:18
Kum 4:12, 13
- l Kut 20:18
Ebr 12:18, 19
- m Kut 24:17

Safu ya 2

- a Kum 4:33, 36
- b Kut 20:19
Ebr 12:18, 19
- c Kum 18:16, 17
- d Kum 10:12
Ayu 28:28
Met 1:7
Mt 10:28
1Pe 2:17
- e Met 4:4
Met 7:2
Mhu 12:13
Isa 48:18
1Yo 5:3
- f Zb 19:8, 11
Yak 1:25
- g Kum 6:3, 25
Kum 8:1
- h Kum 12:32
Yos 1:7, 8

na mwanadamu na mwanadamu huyo aendelee kuishi.^a

25 Sasa, kwa nini tufe? Kwa maana moto huu mkubwa unaweza kututeketeza. Tukiendelea kuisikia sauti ya Yehova Mungu wetu, hakika tutakufa. **26** Kwa maana ni nani kati ya wanadamu wote* aliyesikia sauti ya Mungu aliye hai ikiongea kutoka katika moto kama tulivyosikia na bado anaishi? **27** Wewe mwenyewe nenda karibu, usikie yote ambayo Yehova Mungu wetu atasema, nawe ndiwe utakayetuambia mambo yote ambayo Yehova Mungu wetu anakuambia, nasi tutasikiliza na kutenda mambo hayo.^b

28 “Basi Yehova alisikia maneno mliyoniambia, naye Yehova akaniambia, ‘Nimesikia maneno ambayo watu hawa wamekuambia. Mambo yote waliyosema ni sawa.^c

29 Laiti sikuzote wangukuwa na moyo wenye mwelekeo wa kuniogopa^d na kushika amri zangu zote;^e basi mambo yangewaenda vyema wao na wana wao milele!^f **30** Nenda uwaambie hivi: “Rudini kwenye mahema yenu.” **31** Lakini unapaswa kubaki hapa pamoja nami, nami nitakuambia amri zote, masharti, na sheria unazopaswa kuwafundisha na ambazo wanapaswa kushika katika nchi ninayowapa wamiliki.’ **32** Sasa ninyi watu mnapaswa kuwa waangalifu kufanya kama Yehova Mungu wenu alivyowaamuru.^g Msigeuke kwenda kulia wala kushoto.^h **33** Mnapaswa ku-

5:26 *Au “ni nani mwenye mwili wa nyama.”

tembea katika njia yote ambayo Yehova Mungu wenu amewaamuru mfuata,^a ili mwishi na kufanikiwa na kurefusha siku zenu katika nchi mtakayomiliki.^b

6 “Sasa hizi ndizo amri, masharti, na sheria ambazo Yehova Mungu wako ametoa ili ufundishwe, ili uzi-shike unapovuka kuingia katika nchi ambayo utaimiliki, **2** ili umwogope Yehova Mungu wako na kushika sheria zake zote na amri zake ambazo ninakuamuru wewe—wewe na mwana wako na mjukuu wako^c—siku zote za maisha yako, ili uishi muda mrefu.^d **3** Sikilizeni, enyi Waisraeli, na mzishike kwa uangalifu, ili mfanikiwe na kuwa wengi sana katika nchi inayotiririka maziwa na asali, kama Yehova, Mungu wa mababu zenu, alivyowaahidi.

4 “Sikilizeni, enyi Waisraeli: Yehova Mungu wetu ni Yehova mmoja.^e **5** Ni lazima umpende Yehova Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi^f yako yote na kwa nguvu zako zote.^g **6** Maneno haya ninayokuamuru leo lazima yawe moyoni mwako, **7** nawe lazima uyakazie* kwa wanao^h na kuongea kuyahusu unapoketi nyumbani mwako na unapotembea barabarani na unapolala na unapoamka.ⁱ **8** Yafunge yawe kumbukumbu mkononi mwako, na lazima yawe kama utepe kwenye paji la uso wako.^j **9** Yaandike kwenye miimo ya milango

6:5 *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au “uwezo wako wote.” 6:7 *Au “uyarudie; uyasisitize.” 6:8 *Tnn., “katikati ya macho yako.”

SURA YA 5

a Kum 10:12

b Kum 4:40
Kum 12:28
Ro 10:5

SURA YA 6

c Mwa 18:19
Kum 4:9

d Met 3:1, 2

e Kum 5:7
Isa 42:8
Zek 14:9
Mk 12:29, 32
IKo 8:6f Kum 10:12
Kum 11:13
Kum 30:6
Mt 22:37g Mk 12:30, 33
Lu 10:27h Mwa 18:19
Kum 4:9
Met 22:6
Efe 6:4

i Kum 11:19

j Kum 11:18

Safu ya 2

a Mwa 15:18

b Yos 24:13
Zb 105:44

c Kum 8:10

d Amu 3:7

e Kum 10:12
Kum 13:4

f Lu 4:8

g Yer 12:16

h Kut 34:14

i Kut 20:5
Kum 4:24j Kut 32:9, 10
Hes 25:3
Kum 11:16, 17
Amu 2:14

k 2Fa 17:18

l Mt 4:7
Lu 4:12
IKo 10:9m Kut 17:2, 7
Zb 95:8, 9
Ebr 3:8, 9

n Mwa 15:18

ya nyumba yako na kwenye malango yako.

10 “Yehova Mungu wenu atakapowaleta katika nchi aliyowaapia mababu zenu Abrahamu, Isaka, na Yakobo kwamba atawapa ninyi^a—majiji makubwa na yenye kupe-ndeza ambayo hamkujenga,^b **11** nyumba zilizojaa vitu vizuri vya aina mbalimbali ambavyo hamkufanya kazi ili kuvipata, visima ambavyo hamkuchimba, na mashamba ya mizabibu na mizeituni ambayo hamkupanda—nanyi mtakapokuwa mmekula na kushiba,^c **12** jihadharini msimsahau Yehova,^d aliyewatoa nchini Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa. **13** Mnapaswa kumwogopa^e Yehova Mungu wenu, mnapaswa kumtumikia yeye,^f nanyi mnapaswa kuapa kwa jina lake.^g **14** Msifuata miungu mingine, miungu yoyote ya mataifa yote yanayowazunguka,^h **15** kwa maana Yehova Mungu wenu ambaye yuko miongoni mwenu ni Mungu anayetaka watu wamwabadu yeye peke yake.ⁱ Msipofanya hivyo, hasira ya Yehova Mungu wenu itawaka dhidi yenu,^j naye atawaangamiza kabisa kutoka duniani.^k

16 “Msimjaribu Yehova Mungu wenu kama mlivyomjaribu^l kule Masa.^m **17** Mnapaswa kuzishika kwa bidii amri za Yehova Mungu wenu na vikumbusho vyake na masharti yake ambayo amewaamuru mshike. **18** Ni lazima mfanye mambo mema na yanayofaa machoni pa Yehova, ili mfanikiwe na ili mwingie na kuimiliki nchi nzuri ambayo Yehova aliyawaapia mababu zenu,ⁿ **19** kwa kuwafukuza

maadui wenu wote kutoka mbele yenu, kama Yehova alivyoahidi.^a

20 “Wakati ujao, mwana wako akikuuliza, ‘Vikumbusho, masharti, na sheria* ambazo Yehova Mungu wetu ametuamuru tushike zinamaanisha nini?’ **21** ndipo utakapomwambia mwana wako, ‘Tulikuwa watumwa wa Farao kule Misri, lakini Yehova alitoutoa Misri kwa mkono wenyewe nguvu. **22** Basi mbele ya macho yetu, Yehova aliendelea kufanya ishara na miujiza mikubwa na iliyoleta uharibifu nchini Misri,^b na pia kwa Farao na nyumba yake yote.^c **23** Naye akatutoa huko ili atulete hapa na kutupatia nchi ambayo aliwaapia mababu zetu.^d **24** Kisha Yehova akatuamuru tufuate masharti hayo yote na kumwogopa Yehova Mungu wetu ili tufanikiwe daima,^e na ili tuendele kuishi,^f kama ilivyo leo. **25** Tukimti Yehova Mungu wetu kwa kushika kwa uangalifu amri hizo zote, kama alivyotumuru, tutakuwa waadilifu.^g

7 “Yehova Mungu wenu atakapowaleta katika nchi mnyakaribia kuingia na kumiliki,^h atayaondoa pia mataifa makubwa kutoka mbele yenu:ⁱ Wahiti, Wagirgashi, Waamori,^j Wakanaani, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi,^k mataifa saba makubwa zaidi na yenye nguvu kuliko ninyi.^l **2** Yehova Mungu wenu atawatia watu hao mikononi mwenu, nanyi mtawashinda.^m Mnapaswa kuwaangamiza kabisa.ⁿ Msifanye agano lolote

6:20 *Tnn., “maamuzi ya hukumu.”

SURA YA 6

a Kut 23:30

b Kut 7:3

c Kum 4:34

d Kut 13:5
Kum 1:8e Zb 111:10
Met 14:27f Law 18:5
Kum 4:1
Gal 3:12g Mhu 12:13
Ro 10:5

SURA YA 7

h Kum 31:3

i Kut 33:2
Yos 3:10

j Mwa 15:16

k Mwa 10:15-17

l Kum 20:1

m Hes 33:52

n Law 27:29
Yos 6:17
Yos 10:28

Safu ya 2

a Kut 23:32
Kut 34:15
Kum 20:16, 17b Yos 23:12, 13
1Fa 11:1, 2
Ezr 9:2c Kut 34:16
1Fa 11:4

d Kum 6:14, 15

e Kut 23:24
Kut 34:13

f Kum 16:21, 22

g Kum 7:25
Kum 12:2, 3h Kut 19:5, 6
Kum 14:2
Amo 3:2

i Kum 10:15

j Kum 10:22

k Mwa 22:16, 17

l Kut 6:6
Kut 13:3, 14

pamoja nao wala kuwahurumia.^a **3** Msioane nao kamwe. Msikubali mabinti wenu wao-lewe na wana wao wala msikubali wana wenu wawaoe mabinti wao.^b **4** Kwa maana watawapotosha wana wenu waache kumfuata Mungu na kuanza kuabudu miungu mingine;^c kisha hasira ya Yehova itawaka dhidi yenu, naye ata-waangamiza upesi.^d

5 “Lakini hivi ndivyo mta-kavyowatendea Bomoeni madhabahu zao, vunjeni nguzo zao takatifu,^e kateni miti yao mitakatifu,^{*f} na kuteketeza sanamu zao za kuchongwa.^g

6 Kwa maana ninyi ni watu watakatifu kwa Yehova Mungu wenu, na Yehova Mungu wenu amewachagua ninyi muwe watu wake, mali yake ya pekee,^{*h} kutoka kati ya mataifa yote yaliyo duniani.^h

7 “Yehova hakuwependa na kuwachagua ninyi eti kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote,ⁱ kwa maana mlikuwa taifa dogo zaidi kati ya mataifa yote.^j **8** Badala yake, ni kwa sababu Yehova anawependa na alitimi-za kiapo alichowaapia mababu zenu,^k ndiyo maana Yehova aliwatoa Misri kwa mkono wake wenye nguvu na kuwa-komboa kutoka katika nyumba ya utumwa,^l kutoka katika nguvu za* Farao mfalme wa Misri. **9** Mnajua vizuri kwamba Yehova Mungu wenu ndiye Mungu wa kweli, Mungu mwaminifu, anayetimiza agano lake na kutenda kwa upendo mshikamanifu kufi-

7:5 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 7:6

*Au “mali yake anayothamini sana.”

7:8 *Tnn., “kutoka mikononi mwa.”

kia kizazi cha elfu cha wale wanaompenda na kushika amri zake.^a **10** Lakini wale wanaomchukia atawalipa waziwazi* kwa kuwaangamiza.^b Hatakawia kuwaadhibu wale wanaomchukia; atawalipa waziwazi.* **11** Kwa hiyo, muwe waangalifu kushika amri na masharti na sheria ambazo* ninawaamuru leo, kwa kuzifuata.

12 “Mkiendelea kusikiliza sheria hizi na kuzifuata na kuzitekeleza, Yehova Mungu wenu atatimiza lile agano na kuwatendea kwa upendo mshikamanifu kama alivyowaapia mababu zenu. **13** Atawapenda na kuwabariki na kuwafanya mwongezeke. Naam, atawabariki kwa kuwapa watoto wengi,*^c mazao ya ardhi yenu, nafaka yenu, divai yenu mpya, mafuta yenu,^d ndama na wanakondoo wa makundi yenu, katika nchi aliyowaapia mababu zenu kwamba atawapa ninyi.^e **14** Mtabarikiwa kuliko mataifa mengine yote;^f haku-na mwanamume au mwana-mke yeyote miongoni mweni atakayekosa mtoto, wala mifugo yenu haitakosa kuzaa.^g **15** Yehova atawaondolea magonjwa yote, naye hatawaletea ugonjwa wote unaotisha mliujua kule Misri.^h Badala yake, atawaletea magonjwa hayo wote wanaomchukia. **16** Mtayaangamiza* mataifa yote ambayo Yehova Mungu wenu atayatia mikononi mwenu.ⁱ Msiwahuru-

7:10 *Tnn., “mbele ya uso wao.” 7:11 *Tnn., “maamuzi ya hukumu ambayo.” 7:13 *Tnn., “atabariki uzao wa tumbo lenu.” 7:16 *Tnn., “Mtayameza.”

SURA YA 7

a Kut 34:6, 7

b Met 2:22
2Pe 3:7

c Law 26:9

d Law 26:4

e Mwa 13:14, 15

f Kum 33:29
Zb 147:20g Kut 23:26
Kum 28:11
Zb 127:3

h Kum 28:15, 27

i Kum 7:1, 2
Kum 20:16
Yos 10:28

Safu ya 2

a Mwa 15:16
Law 18:25
Kum 9:5

b Kut 20:3

c Kut 23:33
Kum 12:30
Amu 2:2, 3
Zb 106:36

d Hes 13:31

e Kum 1:29
Kum 31:6
Zb 27:1
Isa 41:10

f Kut 14:13

g Ne 9:10, 11
Yer 32:20

h Kum 4:34

i Kut 23:28
Yos 3:10j Kut 23:29
Kum 2:25
Yos 2:9
Yos 24:12

k Hes 14:9

l Kum 10:17
1Sa 4:7, 8

m Kut 23:30

n Kum 9:3

o Yos 10:24
Yos 12:1

mie*^a kamwe, nanyi msiabudu kamwe miungu yao,^b kwa sababu jambo hilo litakuwa mtego kwenu.^c

17 “Mkijiambia mioyoni mwenu, ‘Mataifa haya yana watu wengi kuliko sisi. Tunawezaje kuyafukuza?’^d **18** msiwaogope.^e Mnapaswa kujikumbusha mambo ambayo Yehova Mungu wenu alimtendea Farao na nchi yote ya Misri,^f **19** zile hukumu kubwa* ambazo mli-ona kwa macho yenu na ishara na miujiza^g na mkono wenye nguvu na mkono ulio-nyooshwa ambao Yehova Mungu wenu alitumia kuwatoa huko.^h Hivyo ndivyo Yehova Mungu wenu atakavyoyatendea mataifa yote mnayoyaogopa.ⁱ **20** Yehova Mungu wenu atawafanya wavunjike moyo* mpaka watakapoangamia wale waliobaki/ na walio-kuwa wakijificha ili msiwagate. **21** Msishtuke kwa sababu yao, kwa maana Yehova Mungu wenu yuko pamoja nanyi,^k Mungu mkuu na mwenye kuogopesha.^l

22 “Kwa hakika Yehova Mungu wenu atayafukuza mataifa haya kutoka mbele yenu kidogo kidogo.^m Hamtaruhusiwa kuwaangamiza upe- si, ili wanyama wa mwituni wasiongezeke na kuwashambulia ninyi. **23** Yehova Mungu wenu atayatia mikononi mwenu na kuyashinda kabisa mpaka yaangamie.ⁿ **24** Atawatia wafalme wa mataifa hayo mikononi mwenu,^o nanyi

7:16 *Tnn., “Jicho lenu lisiwahurumie.” 7:19 *Au “yale majaribu makubwa.” 7:20 *Au labda, “washikwe na wasiwasisi; waogope.”

mtayafutilia mbali majina yao kutoka duniani.*^a Hakuna mtu atakayewazuia,^b mpaka mta- kapowaangamiza.^c **25** Mnapaswa kuchoma moto sanamu kwa kuchongwa za miungu yao.^d Msitamani fedha na dhahabu ya sanamu hizo wala msiichukue,^e ili isiwe mtego kwenu, kwa maana ni chukizo kwa Yehova Mungu wenu.^f **26** Msilete ndani ya nyumba zenu kitu kinachochukiza kwa sababu mtakuwa kama kitu hicho kinachopaswa kuharibiwa. Mnapaswa kukichukia kabisa na kukikirihia kabisa, kwa sababu ni kitu kinachopaswa kuharibiwa.

8 “Mnapaswa kuwa waanga- lifu kushika kila amri ni- nayowapa leo, ili mwendelee kuishi, mwongezeke,^g mwingie na kuimiliki nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zenu.^h **2** Kumbukeni njia ndefu ambayo Yehova Mungu wenu alifanya mtembee nyikani kwa miaka hii 40,ⁱ ili awanyenyekeze na kuwajaribu/ ili ajue yaliyokuwa mioyoni mwenu,^k aone kama mngelizhika amri zake au la. **3** Kwa hiyo aliwanyenyekeza na kuwacha mkae njaa,^l naye akawali- sha mana,^m ambayo ninyi wala baba zenu hamkuwa mmei- jua, ili awafundishe kwamba mwanadamu haishi kwa mka- te tu bali huishi kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Yehova.ⁿ **4** Nguo mlizo- vaa hazikuchakaa, wala miguu yenu haikuvimba miaka hiyo 40.^o **5** Mnajua vizuri mioyo- ni mwenu kwamba kama baba anavyomrekebisha mwana wake, ndivyo Yehova Mu-

7:24 *Tnn., “kutoka chini ya mbingu.”

SURA YA 7

a Kut 17:14
Zb 9:5

b Kum 11:25
Yos 1:5
Ro 8:31

c Yos 11:14

d Kum 12:3
1Nya 14:12

e Isa 30:22

f Kum 27:15

SURA YA 8

g Met 3:1, 2

h Mwa 15:18

i Kum 2:7

j Kut 16:4
Kut 20:20

k Kum 13:3
Met 17:3

l Kut 16:3

m Kut 16:31
Zb 78:24

n Mt 4:4

o Kum 29:5
Ne 9:21

Safu ya 2

a Met 3:12
1Ko 11:32
Ebr 12:5-7
Ufu 3:19

b Kut 3:8
Law 26:4
Kum 11:11, 12

c Hes 13:23

d Eze 20:6

e Kum 6:10-12

f Ho 13:6

g Kum 9:4
Kum 32:15

h Zb 106:21

ngu wenu alivyokuwa akiwa- rekebisha.^a

6 “Basi ni lazima mshike amri za Yehova Mungu wenu kwa kutembea kati- ka njia zake na kumwogopa yeye. **7** Kwa maana Yehova Mungu wenu anawaleta kati- ka nchi nzuri,^b nchi yenye vi- jito vya maji, mabubujiko na chemchemi zinazotiririka* ka- tika bonde tambarare na kati- ka eneo lenye milima, **8** nchi yenye ngano na shayiri, na mizabibu, mitini, na mikoma- manga,^c nchi yenye mafu- ta ya zeituni na asali,^d **9** nchi ambayo haitakuwa na upungufu wa chakula na ha- mtakosa chochote, nchi yenye mawe yaliyo na chuma na ka- tika milima yake mtachimba shaba.

10 “Baada ya kula na kushi- ba, mnapaswa kumsifu Yeho- va Mungu wenu kwa sababu ya nchi nzuri ambayo amewa- pa.^e **11** Jihadharini msimsa- hau Yehova Mungu wenu kwa kutoshika amri zake, maagi- zo yake, na sheria zake ambazo ninawaamuru leo. **12** Baada ya kula na kushi- ba na kujenga nyumba nzu- ri na kukaa humo,^f **13** ng'o- mbe wenu na kondoo wenu watakapokuwa wameongeze- ka na fedha yenu na dhahabu yenu itakapokuwa imeongeze- ka na mtakapokuwa na wingi wa vitu vyote, **14** msiache mioyo yenu iwe na kiburi^g na kuwafanya mumsahau Yehova Mungu wenu, aliyewatoa nchi- ni Misri, kutoka katika nyu- mba ya utumwa,^h **15** aliye- wafanya mtembee katika nyi-

8:7 *Au “vyanzo vya maji vyenye kina kirefu.”

ka kubwa na yenye kutisha,^a iliyo na nyoka wenye sumu na nge na ardhi iliyokauka isiyu na maji. Alifanya maji yatiririke kutoka katika mwamba mgumu^b 16 na kuwalisha mana^c nyikani, ambayo baba zenu hawakuwa wamejua, ili awanyenyekeze^d na kuwajaribu ili awanufaishe baadaye.^e 17 Mkijiambia mioyoni mwenu, 'Nimepata utajiri huu kwa nguvu zangu mwenyewe na uwezo wa mkono wangu mwenyewe,'^f 18 kumbukeni kwamba Yehova Mungu wenu ndiye anayewapa nguvu za kupata utajiri,^g ili atimize agano lake ambalo aliwaopia mababu zenu, kama ilivyo leo.^h

19 "Ikiwa mtamsahau Yehova Mungu wenu na kufuata miungu mingine na kuiabudu na kuiinamia, nashuhudia dhidi yenu leo kwamba hakika mtaangamia.ⁱ 20 Mtaangamia kama mataifa ambayo Yehova anayaangamiza mbele yenu, kwa sababu hamkuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu.^j

9 "Sikilizeni, enyi Waisraeli, leo mnavuka Yordani^k na kuingia kumiliki nchi yenye mataifa makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko ninyi,^l majiji makubwa na yenye ngome zinazofika mbinguni,^m 2 watu wenye nguvu na warefu, wana wa Waanaki,ⁿ mnaowajua na ambao mmesikia watu wakisema hivi kuwahu: 'Ni nani anayeweza kuwashinda wana wa Anaki?' 3 Kwa hiyo, mnapaswa kujua leo kwamba Yehova Mungu wenu atawatangulia mnapo-

9:1 *Yaani, yana kuta ndefu sana.

SURA YA 8

a Kum 1:19

Yer 2:6

b Hes 20:11

c Kut 16:35

d Kum 8:2

e Ebr 12:11

f Ho 12:8

g Kum 7:12

h Zb 127:1

Ho 2:8

i Kum 4:25, 26

Kum 30:17, 18

Yos 23:12, 13

j Da 9:11, 12

SURA YA 9

k Yos 4:19

l Kum 7:1

m Hes 13:28

n Hes 13:33

Safu ya 2

a Kum 1:30

Kum 20:4

Kum 31:3

b Kum 4:24

Ebr 12:29

c Kut 23:31

Kum 7:23, 24

d Kum 7:7, 8

Eze 36:22

e Mwa 15:16

Kum 12:31

Kum 18:9, 12

f Law 18:25

g Mwa 13:14, 15

Mwa 17:1, 8

h Mwa 26:3

i Mwa 28:13

j Kut 34:9

Zb 78:8

k Kum 9:22

Zb 78:40

Ebr 3:16

l Kut 17:2

Hes 11:4

Hes 16:1, 2

Hes 25:2, 3

Kum 31:27

m Kut 32:4, 10

n Kut 24:12

Kut 31:18

Kut 32:16

o Kut 24:7

vuka.^a Yeye ni moto unaoteke-teza,^b atawaangamiza. Atawa-shinda mbele ya macho yenu ili mwafukuze* na kuwaangamiza haraka, kama Yehova alivyoahidi.^c

4 "Yehova Mungu wenu atakapowafukuza kutoka mbele yenu, msiseme hivi mioyoni mwenu: 'Yehova amenileta ili nimiliki nchi hii kwa sababu ya uadilifu wangu mwenyewe.'^d Badala yake, Yehova anayafukuza mataifa hayo^e kutoka mbele yenu kwa sababu ya uovu wao. 5 Hamwendi kumiliki nchi yao kwa sababu ya uadilifu wenu au unyoofu wa mioyo yenu. Badala yake, Yehova Mungu wenu anayafukuza mataifa hayo kutoka mbele yenu^f kwa sababu ya uovu wao na ili Yehova atimize neno alilowaopia mababu zenu, Abrahamu,^g Isaka,^h na Yakobo.ⁱ 6 Basi, mjue kwamba Yehova Mungu wenu hawapi nchi hii nzuri mwiliki kwa sababu ya uadilifu wenu; kwa maana ninyi ni watu wakaidi.*^j

7 "Kumbukeni, msisahau kamwe jinsi mliyomkasirisha Yehova Mungu wenu nyikani.^k Tangu siku mliyotoka nchini Misri mpaka mlipofika mahali hapa, mmekuwa mki-mwasi Yehova.^l 8 Hata kule Horebu mlimkasirisha Yehova, na Yehova akapandwa na hasira sana hivi kwamba alitaka kuwaangamiza.^m 9 Nilipopanda mlimani ili kupokea yale mabamba ya mawe,ⁿ mabamba ya agano ambalo Yehova alifanya pamoja nanyi,^o nilikaa mlimani siku 40

9:3 *Au "mchukue nchi yao." 9:6 *Tnn., "wenye shingo ngumu."

mchana na usiku,^a sikula chakula wala kunywa maji.

10 Kisha Yehova akanipa yale mabamba mawili ya mawe ya liyoandikwa kwa kidole cha Mungu, nayo yalikuwa na maneno yote ambayo Yehova aliwaambia mlimani kutoka katika moto siku ya kusanyiko.*^b

11 Mwishoni mwa zile siku 40 mchana na usiku, Yehova alinipa yale mabamba mawili ya mawe, yale mabamba ya agano, **12** na Yehova akaniaambia, 'Ondoka, shuka upesi kutoka hapa, kwa sababu watu wako uliowatoa Misri wametenda mambo mapotovu.^c Wamegeuka upesi kutoka katika njia niliyowaamuru wafuate. Wamejitengenezea sanamu ya chuma.'^{*d}

13 Kisha Yehova akaniaambia, 'Nimewatazama watu hawa, nikaona ni watu wakaidi.*^e **14** Niche, nami nitawaangamiza na kufutilia mbali jina lao kutoka duniani,* na acha nikufanye wewe kuwa taifa lenye nguvu zaidi na lenye watu wengi kuliko wao.'^f

15 "Basi nikageuka na kushuka mlimani huku mlima ukiwaka moto,^g nami nilikuwa nimebeba yale mabamba mawili ya agano kwa mikono yangu miwili.^h **16** Kisha nikatazama na kuona kwamba mlikuwa mmentendea dhambi Yehova Mungu wenu! Mlikuwa mmejitengenezea ndama wa chuma.* Mlikuwa mmegeuka upesi kutoka katika njia ambayo Yehova alikuwa amewaamuru mfuatē.ⁱ

9:10 *Au "kukutanika." 9:12 *Au "sanamu ya kuyeyushwa." 9:13 *Au "wenye shingo ngumu." 9:14 *Tnn., "kutoka chini ya mbingu." 9:16 *Au "kuyeyushwa."

SURA YA 9

a Kut 24:18

b Kut 19:19
Kum 4:10-13

c Kut 32:7

d Kut 32:4

e Kut 32:9

f Kut 32:10

g Kut 19:18

h Kut 32:15

i Kut 20:3, 4

Safu ya 2

a Kut 32:19

b Kut 34:28

c Kut 32:10

d Kut 32:11, 14
Zb 106:23

e Kut 32:2, 21

f Kut 32:4

g Kut 32:20

h Hes 11:3

i Kut 17:7

j Hes 11:4, 34

k Hes 13:26

l Hes 14:3, 4

m Kum 1:32
Zb 106:24, 25
Ebr 3:19

n Kut 34:28

17 Basi nikashika yale mabamba mawili na kuyatupa chini kwa mikono yangu miwili na kuyavunja mbele ya macho yenu.^a **18** Kisha nikalala kifudufudi mbele za Yehova kwa siku 40, mchana na usiku, kama nilivyofanya mwanzoni. Sikula chakula wala kunywa maji,^b kwa sababu ya dhambi zote mlizokuwa mmentenda kwa kufanya uovu machoni pa Yehova na kumkasirisha. **19** Kwa maana niliogopa sana kwa sababu Yehova alikuwa amewakasirikia sana,^c naye alitaka kuwaangamiza. Hata hivyo, Yehova alinikiliza wakati huo pia.^d

20 "Yehova alimkasirikia sana Haruni hivi kwamba alitaka kumwangamiza,^e lakini wakati huo niliomba dua kwa ajili ya Haruni pia. **21** Halafu nikachukua kile kitu cha dhambi mlichokitengeneza, yule ndama,^f na kumteketeza kwa moto; nikamponda na kumsagasaga kabisa mpaka akawa laini kama mavumbi, nami nikayatupa mavumbi hayo katika kijito kinachotiririka kutoka mlimani.^g

22 "Pia, mlimkasirisha Yehova kule Tabera,^h kule Masa,ⁱ na Kibroth-hataava.^j **23** Yehova alipowatuma kutoka Kadesh-barnea^k na kuwaambia, 'Pandeni mwimiliki nchi ambayo kwa hakika nitawapa!' mliasi tena agizo la Yehova Mungu wenu,^l nanyi hamkuonyesha imani^m kumwelekea wala hamkumtii. **24** Mmekuwa mkimwasi Yehova tangu nilipowajua.

25 "Kwa hiyo niliendelea kulala kifudufudi mbele za Yehova siku 40, mchana na usiku,ⁿ nililala kifudufudi kwa sa-

babu Yehova alisema atawaangamiza. **26** Nikaanza kutoa dua kwa Yehova na kusema, 'Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, usiwaangamize watu hawa. Wao ni mali yako binafsi,*^a watu uliowakomboa kwa ukuu wako na kuwatoa Misri kwa mkono wenye nguvu.^b **27** Wakumbuke watumishi wako Abrahamu, Isaka, na Yakobo.^c Usikazie fikira ukaidi wa watu hawa, uovu wao, na dhambi yao.^d **28** Kama si vyo watu wa nchi ulimotutoa huenda wakasema: "Yehova alishindwa kuwaingiza katika nchi aliyowaahidi, na kwa sababu aliwachukia, aliwatoa ili awaue nyikani."^e **29** Kwa maana ni watu wako na mali yako binafsi,*^f watu uliowatoa kwa nguvu zako kuu na kwa mkono wako ulionyooshwa.^g

10 "Wakati huo Yehova aliniambia, 'Jichongee mabamba mawili ya mawe kama yale ya kwanza,^h upande uje kwangu mlimani; jitengezee pia sanduku la mbao. **2** Nami nitaandika kwenye mabamba hayo maneno yaliyokuwa kwenye yale mabamba ya kwanza ambayo uliyavunja, na uweke mabamba hayo ndani ya sanduku hilo.' **3** Kwa hiyo nikatengeneza sanduku kwa mbao za mshita na kuchonga mabamba mawili ya mawe kama yale ya kwanza na kupanda juu mlimani nikiwa nimebeba mabamba hayo mawili mkononi mwangu.ⁱ **4** Kisha akaandika kwenye mabamba hayo maneno aliyoandika mwanzoni,^j zile Amri Kumi,*^k ambazo Ye-

9:26, 29 *Au "urithi wako." 10:4 *Tnn., "yale Maneno Kumi."

SURA YA 9

a Kut 19:5
Zb 135:4

b Kut 32:11

c Kut 3:6
Kut 6:8
Kum 9:5

d Kut 32:31, 32

e Kut 32:12
Hes 14:15, 16

f 1Fa 8:51
Ne 1:10

g Kut 6:6
Kum 4:20, 34

SURA YA 10

h Kut 34:1

i Kut 34:4

j Kut 32:15

k Kut 20:1
Kut 34:28
Kum 4:13

Safu ya 2

a Kum 4:36
Kum 5:4

b Kut 19:17
Kum 5:22

c Kut 34:29

d Hes 20:23, 24
Hes 33:31, 38

e Hes 20:28

f Hes 33:33

g Hes 1:50
Hes 3:6
Hes 8:14

h Hes 3:30, 31

i Hes 6:23-27
Kum 21:5
2Nya 30:27

j Hes 18:20, 24
Kum 18:1

k Kut 24:18
Kut 34:28

l Kut 32:14

m Mwa 15:18

n Mik 6:8

hova aliwaambia mlimani kutoka katika moto^a siku ya kusanyiko;*^b Yehova akanipa mabamba hayo. **5** Basi nika geuka na kushuka kutoka mlimani^c na kuyaweka mabamba hayo katika sanduku nililokuwa nimetengeneza, na yangali humo, kama Yehova alivyo kuwa ameniamuru.

6 "Kisha Waisraeli wakao ndoka Beerothi Bene-yaakani na kwenda Mosera. Haruni akafa na kuzikwa huko,^d na Eleazari mwana wake akaanza kutumikia akiwa kuhani baada yake.^e **7** Kutoka huko wakaelekea Gudgoda, na kutoka Gudgoda wakaelekea Yotbata,^f nchi yenye vijito vingi vya maji.

8 "Wakati huo Yehova aliliteua kabila la Lawi^g ili libebe sanduku la agano la Yehova,^h lisimame mbele za Yehova ili kumhudumia, na kubariki katika jina lake,ⁱ kama linavyofanya mpaka leo. **9** Ndio maana Lawi hajapewa fungu wala urithi pamoja na ndugu zake. Yehova ndiye urithi wake, kama Yehova Mungu wako alivyokuwa amemwambia.^j **10** Mimi mwenyewe nilika mlimani siku 40, mchana na usiku,^k kama nilivyofanya mwanzoni, na Yehova aliniskiliza wakati huo pia.^l Yehova hakutaka kuwaangamiza. **11** Kisha Yehova akaniambia, "Tangulia mbele ya watu, na mjitayarisha kuondoka, ili waingie na kuimiliki nchi ambayo nimewaapia mababu zao kwamba nitawapa."^m

12 "Sasa, enyi Waisraeli, Yehova Mungu wenu anataka mfanye nini?ⁿ Hili tu ndilo

10:4 *Au "kukutanika."

analotaka: mmwogope Yehova Mungu wenu,^a mtembee katika njia zake zote,^b mumpende, na kumtumikia Yehova Mungu wenu kwa moyo wenu wote na kwa nafsi* yenu yote,^c **13** na kushika amri na sheria za Yehova ninazowaamuru leo kwa faida yenu wenyewe.^d **14** Tazameni, mbingu, hata mbingu za mbingu* ni mali ya Yehova Mungu wenu, pamoja na dunia na vitu vyote vilivyomo.^e **15** Lakini Yehova aliwakaribia na kudhihirisha upendo wake kwa mababu zenu tu, naye amewachagua ninyi, wazao wao,^f kutoka kati ya mataifa yote, kama mlivyo leo. **16** Ni lazima sasa msafishe*^g mioyo yenu na kuacha ukaidi.^h **17** Kwa maana Yehova Mungu wenu ni Mungu wa miunguⁱ na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, mwenye nguvu, na mwenye kuogopesha, asiyempendelea yeyote/na hakubali rushwa. **18** Hu-tekeleza haki kwa ajili ya yaima na mjane^k na kumpenda mkaaji mgeni,^l humpa chakula na mavazi. **19** Ni lazima ninyi pia mumpende mkaaji mgeni, kwa maana mlikuwa wakaaji wageni katika nchi ya Misri.^m

20 "Mnapaswa kumwogopa Yehova Mungu wenu, na kumtumikia yeye,ⁿ mnapaswa kushikamana naye, nanyi mnapaswa kuapa kwa jina lake. **21** Yeye Ndiye mnapaswa kumsifu.^o Yeye ni Mungu wenu, ambaye amewafanyia mambo haya makuu

10:12 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
10:14 *Au "mbingu zilizo juu zaidi."
10:16 *Tnn., "mtahiri govi la." *Au "mwache kufanya shingo zenu kuwa ngumu."

SURA YA 10

a Kum 5:29

b Kum 5:33
Yos 22:5c Kum 6:5
Lu 10:27

d Kum 6:24

e 1Nya 29:11
Zb 24:1
Zb 115:16

f Kum 4:37

g Kum 30:6

h Kut 34:9
Kum 9:6
Kum 31:27i Kut 18:11
2Nya 2:5
Zb 97:9j Mdo 10:34
Ro 2:11k Zb 68:5
Yak 1:27l Law 19:10
Kum 24:14
Zb 146:9m Kut 22:21
Law 19:34

n Lu 4:8

o Kut 15:2
Ufu 19:6

Safu ya 2

a 2Sa 7:23

b Mwa 46:27
Kut 1:5
Mdo 7:14

c Mwa 15:1, 5

SURA YA 11

d Kum 6:5
Kum 10:12
Mk 12:30e Kum 8:5
Ebr 12:6f Kum 5:24
Kum 9:26

g Kut 13:3

h Kum 4:34

i Kut 14:23, 28
Ebr 11:29

j Hes 16:1, 32

na yenye kuogopesha mliyo-yaona kwa macho yenu wenyewe.^a **22** Mababu zenu waliposhuka kwenda Misri walikuwa watu* **70**,^b na sasa Yehova Mungu wenu amewafanya muwe wengi kama nyota za mbinguni.^c

11 "Ni lazima mumpende Yehova Mungu wenu^d na kutimiza sikuzote waji-bu wenu kwake, sheria zake, maagizo yake, na amri zake. **2** Mnajua kwamba leo ninazungumza nanyi, si na wana wenu ambao hawajajua wala kuona nidhamu ya Yehova Mungu wenu,^e ukuu wake,^f mko-no wake wenye nguvu^g na mkono wake ulionyooshwa. **3** Hawakuona ishara zake na matendo yake aliyotenda Misri kwa Farao mfalme wa Misri na kwa nchi yake yote;^h **4** wala mambo ali-yatendea majeshi ya Misri, fa-rasi wa Farao na magari yake ya vita, ambayo yalifuni-kwa na maji ya Bahari Nyeku-ndu walipokuwa wakiwafuatia ninyi, na Yehova akawaanga-miza milele.*ⁱ **5** Hawakuona mambo aliyowatendea nyika-ni mpaka mlipofika mahali hapa, **6** wala mambo ali-yowatendea Dathani na Abira-mu, wana wa Eliabu mwana wa Rubeni, dunia ilipofungu-ka na kuwameza wao pamo-ja na familia zao na mahema yao na kila kiumbe aliye hai aliyewafuata, mbele ya macho ya Waisraeli wote.^j **7** Macho yenu wenyewe yameona mate-ndo yote makuu ambayo Yeh-ova alifanya.

8 "Ni lazima mshike amri yote ninayowapa leo, ili muwe

10:22 *Au "nafsi." 11:4 *Au "mpa-ka leo."

imara na kuvuka ili kuimiliki nchi, **9** na ili mwishi muda mrefu^a katika nchi ambayo Yehova aliapa kwamba ange-wapa mababu zenu na uzao wao,^{*b} nchi inayotiririka maziwa na asali.^c

10 "Nchi mnayoenda kumiliki si kama nchi ya Misri mlikotoka, ambako mlikuwa mkipanda mbegu zenu na kuzimwagilia maji kwa mguu wenu,^{*k} kama bustani ya mbo-ga. **11** Lakini nchi mnayokaribia kuvuka kuingia humo ili kuimiliki ni nchi yenye milima na mabonde tambarare.^d Inanyeshwa na maji ya mvua kutoka mbinguni;^e **12** ni nchi inayotunzwa na Yehova Mungu wenu. Macho ya Yehova Mungu wenu yanaitazama daima, kuanzia mwanzo wa mwaka mpaka mwisho wa mwaka.

13 "Na ikiwa mtatii kwa bidii amri zangu ninazowaamuru leo na kumpenda Yehova Mungu wenu na kumtumikia kwa moyo wenu wote na kwa nafsi^{*} yenu yote,^f **14** nitawapa^{*} pia mvua kwa ajili ya nchi yenu katika majira yake, mvua ya vuli na mvua ya masika, nanyi mtakusanya nafaka yenu na divai yenu mpya na mafuta yenu.^g **15** Nami nitaotesha majani katika mashamba yenu kwa ajili ya mifugo yenu, nanyi mtakula na kushiba.^h **16** Jihadharini msiruhusu mioyo yenu ishawishiwe kukengeuka na kuabudu miungu mingine na kuinamia.ⁱ

11:9 *Tnn., "mbegu yao." **11:10** *Yaani, kwa kutumia mfumo fulani uliokanyagwa kwa mguu, labda mfumo unaotumia gurudumu la maji au kwa kuchimba na kufungua mitaro ya maji kwa miguu. **11:13, 18** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **11:14** *Yaani, Mungu.

SURA YA 11

a Kum 4:40
Met 3:1, 2

b Mwa 13:14, 15
Mwa 26:3
Mwa 28:13

c Kut 3:8
Eze 20:6

d Kum 1:7

e Kum 8:7

f Kum 4:29
Kum 6:5
Kum 10:12
Mt 22:37

g Law 26:4
Kum 8:7-9
Kum 28:12
Yer 14:22

h Kum 8:10

i Kum 8:19
Kum 29:18
Ebr 3:12

Safu ya 2

a Kum 28:15, 23
1Fa 8:35, 36
2Nya 7:13, 14

b Kum 8:19

c Met 7:1-3

d Kum 6:6-9
Met 22:6
Efe 6:4

e Kum 4:40
Met 4:10

f Mwa 13:14, 15

g Kum 6:5
Lu 10:27

h Kum 10:20
Kum 13:4
Yos 22:5

i Kut 23:28
Yos 3:10

j Kum 7:1
Kum 9:1, 5

k Yos 14:9

l Mwa 15:18
Kut 23:31

m Kum 7:24
Yos 1:5

17 Kama sivyo, hasira ya Yehova itawaka dhidi yenu, naye atafunga mbingu hivi kwamba mvua haitanyesha^a na ardhi haitazaa mazao yake nanyi mtaangamia upesi kutoka katika nchi nzuri ambayo Yehova anawapa ninyi.^b

18 "Ni lazima uyakazie maneno haya yangu katika moyo wako na nafsi^{*} yako na ku-yafunga kama kumbukumbu kwenye mkono wako, nayo yanapaswa kuwa kama utepe kwenye paji la uso wako.^{*c}

19 Wafundishe watoto wako maneno haya, na kungea kuyahusu unapoketi nyumbani mwako na unapotembea barabarani na unapolala na unapoamka.^d **20** Yaandike kwenye miimo ya milango ya nyumba yako na kwenye malango yako, **21** ili wewe na wana wako mwishi muda mrefu^e katika nchi ambayo Yehova aliapa kwamba ange-wapa mababu zenu,^f sikuzote ambazo mbingu zitakuwa juu ya dunia.

22 "Ikiwa mtaishika kabisa amri hii ninayowapa na kuitekeleza, mkimpenda Yehova Mungu wenu,^g mkitembea katika njia zake zote na kushikamana naye,^h **23** Yehova atayafukuza mataifa haya yote kutoka mbele yenu,ⁱ nanyi mtamiliki nchi ya mataifa makubwa zaidi na yenye watu wengi kuliko ninyi.^j **24** Kila mahali mtakaponyaga kwa mguu wenu patakuwa penu.^k Mpaka wenu utanzia nyikani mpaka Lebanoni, kuanzia ule Mto, mto Efrati, mpaka Bahari ya Mgharibi.^{*l} **25** Hakuna yeyote atakayewazuia.^m

11:18 *Tnn., "katikati ya macho yako." **11:24** *Yaani, ile Bahari Kuu, Mediterania.

Yehova Mungu wenu atawafanya wakaaji wote wa nchi mtakayokanyaga wawahofu na kuwaogopa,^a kama alivyowaahidi ninyi.

26 “Tazameni, leo ninaweka mbele yenu baraka na laana:^b **27** baraka, ikiwa mtatii amri za Yehova Mungu wenu ninazowaamuru ninyi leo,^c **28** na laana, ikiwa hamtatii amri za Yehova Mungu wenu^d na mkigejua kutoka katika njia ninayowaamuru mfuata leo na mkifuata miungu mingine ambayo hamjajua.

29 “Yehova Mungu wenu atakapowaleta katika nchi ambayo mtamiliki, ni lazima mtangaze baraka kwenye Mlima Gerizimu na laana kwenye Mlima Ebali.^e **30** Je, haiko ng’ambo ya Yordani upande wa magharibi,^{*} katika nchi ya Wakanaani wanaoishi Araba, mbele ya Gilgali, kando ya ile miti mikubwa ya More?^f **31** Kwa maana mnavuka Yordani mwingie na kuimiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa ninyi.^g Mtakapoimiliki na kuishi humo, **32** ni lazima muwe waangalifu kutekeleza masharti na sheria zote ninazoweka^{*} mbele yenu leo.^h

12 “Haya ndiyo masharti na sheria ambazo mnapaswa kuwa waangalifu kutekeleza sikuzote mtakazokuwa hai katika nchi ambayo Yehova Mungu wa mababu zenu atawapa mwimiliki. **2** Mnapaswa kuharibu sehemu zote ambazo watu wa mataifa mtakaomiliki nchi yao

11:30 *Au “machweo ya jua.” **11:32** *Tnn., “maamuzi yote ya hukumu ninayoweka.”

SURA YA 11

a Kut 23:27
Yos 2:9,10
Yos 5:1

b Kum 30:15

c Kum 28:1, 2
Zb 19:8, 11

d Law 26:15, 16
Isa 1:20

e Kum 27:12, 13
Yos 8:33, 34

f Mwa 12:6

g Yos 1:11

h Kum 5:32
Kum 12:32

Safu ya 2

SURA YA 12

a Kut 34:13

b Kut 23:24

c Kum 7:25

d Kut 23:13
Yos 23:7

e Law 18:3
Kum 12:31

f 2Nya 7:12

g Law 1:3

h Kum 14:22

i Hes 18:19
Kum 12:11

j 1Nya 29:9
Ezr 2:68

k Kum 12:17
Kum 15:19

l Kum 15:19, 20

m Law 23:40
Kum 12:12, 18
Kum 14:23, 26
Zb 32:11
Zb 100:2
Flp 4:4

n 1Fa 8:56
1Nya 23:25

o Yos 3:17

wamekuwa wakiabudia miungu yao,^a iwe ni juu ya milima mirefu au kwenye vilima au chini ya mti wowote wenye majani mengi. **3** Mnapaswa kubomoa madhabahu zao, kuvunjavunja nguzo zao takatifu,^b kuteketeza kwa moto miti yao mitakatifu,^{*} na kukatakata sanamu za kuchongwa za miungu yao,^c na kuondoa kabisa majina ya miungu yao kutoka sehemu hizo.^d

4 “Hampaswi kumwabudu Yehova Mungu wenu kwa njia hiyo.^e **5** Badala yake, mtafuteni Yehova Mungu wenu mahali popote atakapochagua kuweka jina lake na mahali atakapokaa miongoni mwa makabila yote, mwende mahali hapo.^f **6** Hapo ndipo mnapapaswa kupeleka dhahibu zenu za kuteketezwa,^g matoleo yenu, sehemu zenu za kumi,^h mchango kutoka mkononi mwenu,ⁱ dhahibu zenu za nadhiri, matoleo yenu ya hiariri,^j na wazaliwa wa kwanza wa ng’ombe na kondoo wenu.^k **7** Ni lazima ninyi na familia zenu mle hapo mbele za Yehova Mungu wenu^l na kushangilia katika kazi zenu zote,^m kwa sababu Yehova Mungu wenu amewabariki.

8 “Msifanye kama tunavyofanya hapa leo, kila mtu anafanya jambo analoona ni jema machoni pake mwenyewe,^{*} **9** kwa sababu bado hamjafika mahali pa kupumzikaⁿ na katika urithi ambao Yehova Mungu wenu atawapa. **10** Mtakapovuka Yordani^o na kuishi katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu atawapa ili mwimiliki, kwa hakika atawa-

12:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012. **12:8** *Au “analofikiri linafaa.”

mzisha kutokana na maadui wenu wote wanaowazunguka, nanyi mtakaa kwa usalama.^a

11 Mtaleta vitu vyote ninavyo waamuru mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua jina lake likae hapo^b—dhabihu zenu za kuteketezwa, matoleo yenu, sehemu zenu za kumi,^c mchango kutoka mkononi mwenu, na kila dhabihu ya nadhiri mnayoweka nadhiri kwa Yehova. **12** Mta-shangilia mbele za Yehova Mungu wenu,^d ninyi na wana wenu, binti zenu, watumwa wenu wa kiume na wa kike, na Mlawi yeyote aliye ndani ya majiji* yenu, kwa sababu hajapewa fungu wala urithi pamoja nanyi.^e **13** Jihadharini msitoe dhabihu za kuteketezwa mahali pengine popote mtakapoona.^f **14** Mnapaswa kutoa dhabihu zenu za kuteketezwa mahali tu ambapo Yehova atachagua katika mojawapo ya maeneo ya makabila yenu, na hukio ndiko mtakapofanya yote ninayowaamuru ninyi.^g

15 “Lakini wakati wowote mnapotamani nyama, mtamchinja mnyama na kula nyama yake^h kulingana na baraka ambayo Yehova Mungu wenu amewapa katika majiji* yenu yote. Mtu asiye safi na mtu aliye safi anaweza kula, kama mnavyokula swala au paa. **16** Lakini msile damu kamwe;ⁱ mnapaswa kuimwaga ardhini kama maji.^j **17** Hamtaruhusiwa kula ndani ya majiji* yenu sehemu ya kumi ya nafaka yenu, divai yenu mpya, mafuta yenu, wazaliwa wa kwanza wa ng’ombe na

12:12, 17, 18, 21 *Tnn., “malango.”
12:15 *Tnn., “ndani ya malango.”

SURA YA 12

a Kum 33:28
1Fa 4:25

b Kum 16:2
Kum 26:2

c Kum 14:22, 23

d Kum 14:26
1Fa 8:66
Ne 8:10

e Hes 18:20, 24
Kum 10:9
Kum 14:28, 29
Yos 13:14

f Law 17:3, 4
1Fa 12:28

g 2Nya 7:12

h Kum 12:21

i Mwa 9:4
Law 7:26
Law 17:10
Mdo 15:20, 29

j Law 17:13
Kum 15:23

Safu ya 2

a Kum 14:22, 23

b Kum 12:11
Kum 14:26

c Hes 18:21
Kum 14:27
2Nya 31:4
Ne 10:38, 39
Mal 3:8

d 1Fa 4:21

e Mwa 15:18
Kut 34:24
Kum 11:24

f Law 11:2-4

g Kum 14:23
2Nya 7:12

h Kum 14:4, 5

i Law 3:17
Kum 12:16

j Mwa 9:4
Law 17:11, 14

k Law 17:13
Kum 15:23

kondoo wenu,^a dhabihu yoyote mnayoweka nadhiri, matoleo yenu ya hiari, au mchango kutoka mkononi mwenu. **18** Mnapaswa kula vitu hivyo mbele za Yehova Mungu wenu mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua^b—ninyi na wana wenu, mabinti wenu, watumishi wenu wa kiume na vijakazi wenu, na Mlawi yeyote aliye ndani ya majiji* yenu; nanyi mtashangilia mbele za Yehova Mungu wenu katika kazi zenu zote. **19** Jihadharini msimpuuze Mlawi^c yeyote sikuzote mtakazoishi katika nchi yenu.

20 “Yehova Mungu wenu atakapopanua eneo lenu,^d kama alivyowaahidi,^e nanyi msememe, ‘Nataka kula nyama,’ kwa sababu mnapotamani* kula nyama, mnaweza kula nyama wakati wowote mnapotamani kuila.^f **21** Ikiwa mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua kuweka jina lake^g ni mbali kutoka kwenu, basi mnapaswa kuwachinja baadhi ya ng’ombe wenu au kondoo wenu ambao Yehova amewapa, kama nilivyowaamuru, nanyi mnapaswa kuwala ndani ya majiji* yenu wakati wowote mnapotamani nyama. **22** Mnaweza kuwala kama mnavyokula swala na paa;^h mtu asiye safi na mtu aliye safi anaweza kuila. **23** Ila tu mwazimie kwa uthabiti kutokula damu,ⁱ kwa sababu damu ndiyo uhai,* nanyi hampaswi kula uhai* pamoja na nyama. **24** Msile. Mnapaswa kuimwaga ardhini kama maji.^k **25** Msile, ili mambo yawaendee

12:20 *Au “nafsi zenu zinatamani.”
12:23 *Au “nafsi.”

vyema ninyi na watoto wenu baada yenu, kwa sababu mnafanya lililo sawa machoni pa Yehova. **26** Mnapaswa kuleta tu vitu vitakati-fu ambavyo ni vyenu na dhahihu zenu za nadhiri mnapokuja mahali ambapo Yehova atachagua. **27** Mtatoa mahali hapo dhahihu zenu za kuteketezwa, nyama na damu,^a juu ya madhabahu ya Yehova Mungu wenu, na damu ya dhahihu zenu inapaswa kumwagwa kando ya madhabahu^b ya Yehova Mungu wenu, lakini mna-weza kula nyama.

28 “Muwe waangalifu kutii maneno haya yote ninayowaamuru ninyi, ili mambo yawaendee vyema sikuzote ninyi pamoja na wana wenu baada yenu, kwa sababu mnafanya mambo mema na yaliyo sawa machoni pa Yehova Mungu wenu.

29 “Yehova Mungu wenu atakapoyaangamiza mataifa ambayo mtamiliki nchi yao,^c na mtakapokuwa mkiishi katika nchi yao, **30** jihadhari ni msinaswe baada ya mataifa hayo kuangamizwa kutoka mbele yenu. Msiulize hivi kuhusu miungu yao: ‘Mataifa haya yaliabuduye miungu yake? Mimi pia nitafanya vivyovy hivyo.’^d **31** Msimfanyie hivyo Yehova Mungu wenu, kwa sababu mataifa hayo yanaifanyia miungu yao kila jambo linalochukiza ambalo Yehova anachukia, hata kuwateketeza motoni wana na mabinti wao kwa ajili ya miungu yao.^e **32** Mnapaswa kutenda kwa uangalifu kila neno ninawaamuru.^f Msiongeze wala kupunguza jambo lolote katika maneno hayo.^g

SURA YA 12

a Law 17:11

b Law 4:29, 30

c Kut 23:23
Zb 44:2
Zb 78:55d Kum 7:16
Zb 106:36
Eze 20:28e Law 18:3, 21
Law 20:2
Kum 18:10-12
Yer 32:35

f Yos 22:5

g Kum 4:2
Yos 1:7

Safu ya 2

SURA YA 13

a Isa 8:19
Yer 27:9

b Kum 8:2

c Kum 6:5
Kum 10:12
Mt 22:37

d Kum 10:20

e Kum 18:20

f Kum 17:2, 3, 7
1Ko 5:13g 1Fa 11:4
2Pe 2:1

13 “Ikiwa nabii au mtu ana yebashiri kupitia ndoto atatokea miongoni mwenu na kuwapa ishara au dalili ya ajabu, **2** kisha ishara au dalili hiyo aliyowaambia itimie wakati anaposema, ‘Acheni tui-fuate miungu mingine’, miungu msiojua, ‘na acheni tui-abudu,’ **3** hampaswi kusikiliza maneno ya nabii huyo au mwotaji huyo wa ndoto,^a kwa sababu Yehova Mungu wenu anawajaribu^b ili ajue ikiwa mnampenda Yehova Mungu wenu kwa moyo wenu wote na kwa nafsi* yenu yote.^c

4 Mnapaswa kumuata Yehova Mungu wenu, mnapaswa kumwogopa yeye, mnapaswa kushika amri zake, mnapaswa kuisikiliza sauti yake; yeye ndiye mnayepaswa kumtumikia, nanyi mnapaswa kushikamana naye kabisa.^d **5** Lakini nabii huyo au mwotaji huyo wa ndoto anapaswa kuuawa,^e kwa sababu aliwachochea mmwasi Yehova Mungu wenu — aliyewatoa nchini Misri na kuwakomboa kutoka katika nyumba ya utumwa—ili mtoke katika njia ambayo Yehova Mungu wenu amewaamuru mtembee. Nanyi lazima mwondoe kilicho kiovu kutoka miongoni mwenu.^f

6 “Ikiwa ndugu yako, mwana wa mama yako, au mwana wako au binti yako au mke wako mpendwa au rafiki yako wa karibu sana* atajaribu kukushawishi kwa siri, akisema, ‘Twende tukaabudu miungu mingine,’^g miungu ambayo wewe wala mababu zako hamwijiui, **7** kutoka miongo-

13:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 13:6

*Au “rafiki yako ambaye ni kama nafsi yako mwenyewe.”

ni mwa miungu ya mataifa yanayowazunguka, yaliyo kariibu nanyi au mbali nanyi, kutoka mwisho mmoja wa nchi mpaka mwisho mwingine wa nchi, **8** usikubali ushawishi wake wala kumsikiliza,^a wala usimsikitikie wala kumhurumia wala kumlinda; **9** badala yake, ni lazima umuue.^b Mkonu wako unapaswa kuwa wa kwanza kumuua, kisha mikono ya watu wote itafuata.^c **10** Nawe lazima umuue kwa kumpiga mawe,^d kwa sababu alijaribu kukugeza umwache Yehova Mungu wako, aliyekutoa nchini Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa. **11** Hivyo, Waisraeli wote watasikia na kuogopa, na kamwe hawatafanya tena jambo lolote baya kama hilo miongoni mwenu.^e

12 “Ikiwa mtasikia iki-semwa hivi katika mojawapo ya majiji yenu ambayo Yehova Mungu wenu anawapa mkae humo: **13** ‘Watu wasiofaa kitu wametokea miongoni mwenu ili kuwapotosha wakaaji wa jiji lao, wakisema, “Twendeni tukaabudu miungu mingine,” miungu ambayo hamwijui,’ **14** mnapaswa kupeleleza jambo hilo, kufanya uchunguzi kamili na kuuliza kwa makini;^f na ikithibitishwa ni kweli kwamba jambo hilo lenye kuchukiza limefanywa miongoni mwenu, **15** ni lazima muwaangamize kwa upanga wakaaji wa jiji hilo.^g Mtawaangamiza^h kwa upanga watu wa jiji hilo pamoja na kila kitu kilichomo, kutia ndani mifugo yao. **16** Kisha mtakusanya nyara zote za jiji hilo katikati ya uwanja wa jiji na kuliteketeza jiji hilo

SURA YA 13

a Gal 1:8

b Kut 22:20
Kut 32:27
Hes 25:5

c Kum 17:2, 3, 7

d Law 20:2, 27

e Kum 17:13
1Ti 5:20f Kum 19:15
1Ti 5:19g Kum 17:4, 5
2Nya 28:6

h Kut 22:20

Safu ya 2

a Yos 6:18

b Mwa 22:15, 17
Mwa 26:3, 4

c Kum 6:18

SURA YA 14

d Law 19:28

e Law 21:1, 5

f Law 19:2
Law 20:26
Kum 28:9
1Pe 1:15g Kut 19:5, 6
Kum 7:6h Law 11:43
Law 20:25
Mdo 10:14

i Law 11:2, 3

kwa moto, na nyara hizo zitakuwa dhabihu nzima ya kuteketezwa kwa Yehova Mungu wenu. Nalo litabaki rundo la magofu milele. Halipaswi kamwe kujengwa tena. **17** Mikono yenu haipaswi kuchukua kitu chochote kinachopaswa kuharibiwa,^{*a} ili Yehova aache hasira yake kali na kuwaonyesha rehema na huruma na kuwafanya mwongezeke, kama alivyowaapia mababu zenu.^b **18** Kwa maana mnapaswa kumtii* Yehova Mungu wenu kwa kushika amri zake zote ambazo ninawaamuru leo, na hivyo kufanya yaliyo sawa machoni pa Yehova Mungu wenu.^c

14 “Ninyi ni wana wa Yehova Mungu wenu. Msi-jikatekate^d wala kunyoa upara kwenye mapaji ya nyuso zenu* kwa ajili ya mtu aliyekufa.^e **2** Kwa maana ninyi ni watu watakatifu^f kwa Yehova Mungu wenu, na Yehova amewachagua ninyi muwe watu wake, mali yake ya pekee,* kutoka kati ya mataifa yote duniani.^g

3 “Msile kitu chochote kinachochukiza.^h **4** Hawa ndio wanyama mnaoweza kula: ng'ombe, kondoo, mbuzi, **5** paa, swala, kulungu, mbuzi mwitu, mbawala, kondoo mwitu, na kondoo wa mlimani. **6** Mnaweza kumla mnyama yeyote mwenye kwato zilizopasuka na zilizogawanyika mara mbili na ambaye anacheua. **7** Lakini hampaswi

13:17 *Au “kilichofanywa kitakatifu kwa kupigwa marufuku.” **13:18** *Au “kusikiliza sauti ya.” **14:1** *Tnn., “kutia (kunyoa) upara katikati ya macho yenu.” **14:2** *Au “mali yake anayothamani sana.”

kuwala wanyama wafuatao wanaocheua au wenye kwato zilizogawanyika: ngamia, sungura, na wibari, kwa sababu wanacheua lakini kwato zao hazijapasuka. Wao si safi kwenu.^a **8** Pia, msimle nguruwe kwa sababu ana kwato zilizopasuka lakini hacheui. Yeye si safi kwenu. Msile kamme nyama yao wala kugusa mizoga yao.

9 “Kati ya viumbe wote wanaoishi ndani ya maji, mna-weza kula wafuatao: Mnaweza kumla kiumbe yeyote mwenye mapezi na magamba.^b **10** Lakini hampaswi kumla kiumbe yeyote ambaye hana mapezi na magamba. Yeye si safi kwenu.

11 “Mnaweza kumla ndege yeyote aliye safi. **12** Lakini hampaswi kuwala ndege wafuatao: tai, furukombe, tumbusi mweusi,^{*c} **13** mwewe mwekundu, mwewe mweusi, kila aina ya ndege mbua, **14** kila aina ya kunguru, **15** mbuni, bundi, shakwe, kila aina ya kipanga, **16** bundi mdogo, bundi mwenye masikio marefu, batamaji, **17** mwari, tumbusi, mnanzi, **18** korongo, kila aina ya kulastara, hudihudi, na popo. **19** Pia, kila kiumbe* mwenye mabawa anayeishi katika makundi makubwa si safi kwenu. Hawapaswi kuliwa. **20** Mnaweza kumla kiumbe yeyote safi anayeruka.

21 “Msimle mnyama yeyote aliyepatikana amekufa.^d Mnaweza kumpa mkaaji mgeni aliye ndani ya majiji yenu,^{*} naye anaweza kumla, au mnyama

14:12 *Au “tai mla mizoga.” 14:19 *Au “mdudu.” 14:21 *Tnn., “malango.”

SURA YA 14

a Law 11:4-8

b Law 11:9,10

c Law 11:13-20

d Kut 22:31
Law 17:15

Safu ya 2

a Kut 23:19
Kut 34:26b Kum 12:11
Kum 26:12c Kum 12:5,17
Kum 15:19,20

d Zb 111:10

e Kum 12:5,6

f Kum 12:7
Kum 26:11
Zb 100:2g Hes 18:21
2Nya 31:4
1Ko 9:13h Hes 18:20
Kum 10:9

huyo anaweza kuuzwa kwa mgeni. Kwa maana ninyi ni watu watakatifu kwa Yehova Mungu wenu.

“Msimchemshe mwanambuzi katika maziwa ya mama yake.^a

22 “Ni lazima mtoe sehemu ya kumi ya mazao ya shambani yanayotokana na mbegu zenu mwaka baada ya mwaka.^b **23** Mtakula sehemu ya kumi ya nafaka yenu, divai yenu mpya, mafuta yenu, na wazaliwa wa kwanza wa ng’ombe wenu na kondoo wenu mbele za Yehova Mungu wenu mahali ambapo atachagua jina lake likae hapo,^c ili mji-funze kumwogopa Yehova Mungu wenu sikuzote.^d

24 “Lakini ikiwa safari ni ndefu sana kwenu na hivyo hamwezi kupeleka vitu hivyo mahali ambapo Yehova Mungu wenu amechagua jina lake likae hapo,^e kwa sababu ni mbali sana (kwa sababu Yehova Mungu wenu atawabariki), **25** basi mnaweza kubadilisha vitu hivyo kwa pesa, na mbebe pesa hizo mikononi mwenu na kwenda mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua. **26** Kisha mnaweza kutumia pesa hizo kununua chochote mnachotamani, iwe ni ng’ombe, kondoo, mbuzi, divai na vinywaji vingine vyenye kileo, na kitu chochote mpendacho; nanyi mtakula huko mbele za Yehova Mungu wenu na kushangilia, ninyi na familia zenu.^f **27** Na msimpuuze Mlawi yeyote aliye ndani ya majiji yenu,^g kwa sababu hajapewa fungu wala urithi pamoja nanyi.^h

28 “Mwishoni mwa kila miaka mitatu mnapaswa kuleta

sehemu yote ya kumi ya mazao yenu ya mwaka huo na kuyahifadhi ndani ya majiji yenu.^a **29** Kisha Mlawi, ambaye hajapewa fungu wala urithi kati yenu, mkaaji mgeni, yatima, na mjane aliye ndani ya majiji yenu atakuja kula na kushiba,^b ili Yehova Mungu wenu awabariki katika mambo yote mnayofanya.^c

15 “Mwishoni mwa kila miaka saba mnapaswa kufuta madeni.^d **2** Hivi ndivyo mtakavyoyafuta: Kila mtu aliyemkopesha jirani yake atafuta deni hilo. Hapaswi kudai malipo kutoka kwa jirani au ndugu yake, kwa maana yatatangazwa yamefutwa kwa agizo la Yehova.^e **3** Mnaweza kudai malipo kutoka kwa mgeni,^f lakini mnapaswa kufuta deni lolote la ndugu yenu. **4** Hata hivyo, hakuna yeyote kati yenu anayepaswa kuwa maskini, kwa sababu hakika Yehova atawabariki^g katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa mwimiliki kama urithi, **5** lakini ikiwa tu mtatii kabisa sauti ya Yehova Mungu wenu na kushika kwa uangalifu amri yote hii ninayowapa leo.^h **6** Kwa maana Yehova Mungu wenu atawabariki kama alivyowaahidi, nanyi mtayakopesha mataifa mengi, lakini ninyi hamtahitaji kukopa;ⁱ nanyi mtatawala mataifa mengi, lakini hayatawatawala.^j

7 “Ikiwa mmoja wa ndugu zenu atakuwa maskini miongoni mwenu katika mojawapo ya majiji yaliyo katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, msiiifanye mioyo yenu iwe migumu au kumfumbia mkono ndugu yenu ma-

SURA YA 14

a Kum 26:12

b Kut 22:21
Kum 10:18
Yak 1:27c Kum 15:10
Zb 41:1
Met 11:24
Met 19:17
Mal 3:10
Lu 6:35

SURA YA 15

d Law 25:2

e Kum 31:10

f Kut 12:43
Kum 14:21
Kum 23:20

g Kum 28:8

h Yos 1:7, 8
Isa 1:19

i Kum 28:12

j Kum 28:13
1Fa 4:24, 25

Safu ya 2

a Met 21:13
Yak 2:15, 16
1Yo 3:17b Law 25:35
Met 19:17
Mt 5:42
Lu 6:34, 35
Gal 2:10

c Kum 15:1

d Kut 22:22, 23
Kum 24:14, 15
Met 21:13e Mdo 20:35
2Ko 9:7
1Ti 6:18
Ebr 13:16f Kum 24:19
Zb 41:1

g Mt 26:11

h Met 3:27
Mt 5:42
Lu 12:33i Kut 21:2
Law 25:39

skini.^a **8** Kwa maana mnapaswa kumfumbulia mkono wenu kwa ukarimu^b na kufanya yote mwezayo kumkopesha* chochote anachohitaji au alichopungukiwa. **9** Jiha-dharini wazo hili ovu lisiingie mioyoni mwenu: ‘Mwaka wa saba, mwaka wa kufuta madeni, umekaribia,^c na hivyo mkatae kumtendea kwa ukarimu ndugu yenu aliye maskini na kukosa kumpa chochote. Akimlilia Yehova kuwahu-su ninyi, mtakuwa mmetenda dhambi.^d **10** Mnapaswa kumpa kwa ukarimu,^e nanyi hampaswi* kumpa huku mkinung’unika, kwa sababu hiyo Yehova Mungu wenu atabariki kila kazi na kila jambo mna-lofanya.^f **11** Kwa maana sikuzote kutakuwa na maskini nchini.^g Ndiyo sababu nina-waamuru hivi: ‘Mnapaswa kumfumbulia mkono wenu kwa ukarimu ndugu yenu anayete-seka na maskini katika nchi yenu.’^h

12 “Ikiwa uliuziwa ndugu yako, mwanamume au mwanamke Mwebrania, naye amekutumikia kwa miaka sita, basi katika mwaka wa saba unapaswa kumwachilia huru.ⁱ **13** Na ikiwa utamwachilia huru, usimwache aende mikonomitupu. **14** Mpe kwa ukarimu kitu fulani kutoka katika mifugo yako, uwanja wako wa kupuria, na shinikizo lako la mafuta na divai. Unapaswa kumpa kama vile ambavyo Yehova Mungu wako amekubariki. **15** Kumbuka kwamba ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri na Yehova Mungu wako akakukombo.

15:8 *Au “kumkopesha kwa rehani.”
15:10 *Tnn., “moyo wenu haupaswi.”

Ndiyo sababu leo ninakuamuru ufanye hivyo.

16 “Lakini akikuambia, ‘Sitakuacha!’ kwa sababu anaku-
penda wewe na familia yako,
kwa maana amefuraha kuwa
pamoja nawe,^a **17** utachu-
kua msumari na kutoboa sikio
lake kwa msumari huo mpaka
upenye mlangoni, naye ataku-
wa mtumwa wako daima. Uta-
mfanyia kijakazi wako vivyo
hivyo. **18** Usione vigumu ku-
mwachilia huru, naye aondo-
ke, kwa sababu thamani ya
utumishi wake kwa miaka sita
aliyokutumikia ni mara mbi-
li ya thamani ya utumishi wa
mfanyakazi aliyeajiriwa, na
Yehova Mungu wako ameku-
bariki katika kila jambo
ambalo lilifanywa.

19 “Unapaswa kumtakasa
kila mzaliwa wa kwanza
wa kiume wa ng’ombe wako
na kondoo wako kwa ajili
ya Yehova Mungu wako.^b Usi-
mtumie mzaliwa wa kwanza
wa ng’ombe dume wako kufa-
nya kazi yoyote wala usimkate
manyoya mzaliwa wa kwanza
wa kondoo wako. **20** Wewe
na familia yako mnapaswa ku-
mla mbele za Yehova Mungu
wenu mwaka baada ya mwaka
mahali ambapo Yehova Mungu
wenu atachagua.^c **21** Lakini
ikiwa ana kasoro, yaani, ni
mlemavu, ni kipofu, au ana
kasoro nyingine kubwa, usi-
mtoe dhabihu kwa Yehova Mu-
ngu wako.^d **22** Mnapaswa
kumla ndani ya majiji* yenu,
mtu asiye safi na aliye safi wa-
tamla, kama mnavyokula swa-
la au paa.^e **23** Lakini hampa-
swi kula damu yake;^f mtai-
mwaga ardhini kama maji.^g

15:22 * Tnn., “malango.”

SURA YA 15

a Kut 21:5, 6

b Kut 13:2
Kut 22:30
Hes 3:13
Hes 18:15, 17

c Kum 12:5, 6
Kum 14:23
Kum 16:11

d Law 22:20
Kum 17:1
Mal 1:8
Ebr 9:14

e Kum 12:15
Kum 14:4, 5

f Mwa 9:4
Law 7:26
Mdo 15:20, 29

g Law 17:10, 13
Kum 12:16

Safu ya 2

SURA YA 16

a Kut 12:14
Law 23:5
Hes 9:2
Hes 28:16
1Ko 5:7

b Kut 34:18

c Mt 26:17

d Kut 12:5, 6
2Nya 35:7

e 1Fa 8:29

f Kut 13:3
Law 23:6
Hes 28:17
1Ko 5:8

g Kut 12:33

h Kut 12:14
Kut 13:8, 9

i Kut 12:15
Kut 13:7

j Kut 12:10
Kut 34:25

k Kut 12:3, 6
Hes 9:2, 3
Mt 26:19, 20

l Kut 12:8
2Nya 35:13

m Yoh 2:13
Yoh 11:55

16 “Adhimisheni mwezi wa
Abibu* na msherehe-
kee Pasaka ya Yehova Mu-
ngu wenu,^a kwa sababu ka-
tika mwezi wa Abibu, Yeho-
va Mungu wenu aliwatoa
nchini Misri wakati wa usi-
ku.^b **2** Nanyi mnapaswa ku-
mtolea Yehova Mungu wenu
dhabihu ya Pasaka^c kutoka
katika kondoo wenu na ng’o-
mbe wenu,^d mahali ambapo
Yehova atachagua jina lake li-
kae hapo.^e **3** Hampaswi kula
kitu chochote chenye chachu
pamoja na dhabihu hiyo;^f kwa
siku saba mnapaswa kula mi-
kate isiyo na chachu, mikate
ya mateso, kwa sababu mlito-
ka haraka katika nchi ya Mis-
ri.^g Fanyeni hivyo sikuzote
za maisha yenu ili mkumbu-
ke siku mliyotoka katika nchi
ya Misri.^h **4** Msipatikane na
unga wovote uliokandwa we-
nye chachu katika nchi yenu
yote kwa siku saba,ⁱ wala nya-
ma yoyote mtakayotoa dhabi-
hu siku ya kwanza jioni haipa-
swi kubaki usiku kucha mpa-
ka asubuhi.^j **5** Hamtaruhusi-
wa kutoa dhabihu ya Pasaka
katika jiji lolote tu kati ya ma-
jiji ambapo Yehova anawapa
ninyi. **6** Bali mtafanya hivyo
mahali ambapo Yehova Mu-
ngu wenu atachagua jina lake
likae hapo. Mnapaswa kutoa
dhabihu ya Pasaka wakati wa
jioni mara tu baada ya jua ku-
tua,^k wakati uleule mliotoka
Misri. **7** Mtaipika na kuila^l
mahali ambapo Yehova Mu-
ngu wenu atachagua,^m na asu-
buhi mtarudi kwenye mahema
yenu. **8** Kwa siku sita mta-
kula mikate isiyo na chachu,
na siku ya saba kutakuwa na

16:1 * Angalia Nyongeza B15.

kusanyiko takatifu kwa Yehova Mungu wenu. Hampaswi kufanya kazi yoyote.^a

9 “Mtahesabu majuma saba. Mnapaswa kuanza kuhesabu majuma saba wakati mnapoanza kuvuna kwa mundu nafaka iliyo shambani.^b **10** Kisha mtafanya Sherehe ya Majuma kwa Yehova Mungu wenu^c kwa toleo la hiari linalotoka mkononi mwenu, kulingana na baraka ambazo Yehova Mungu wenu amewapa.^d **11** Nanyi mnapaswa kushangilia mbele za Yehova Mungu wenu, ninyi na wana wenu, mabinti wenu, watumwa wenu wa kiume, vijakazi wenu, Walawi walio ndani ya majiji* yenu, wakaaji wage-ni, mayatima, na wajane walio kati yenu, mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua jina lake likae.^e **12** Kumbuke-ni kwamba mlikuwa watumwa Misiri,^f nanyi mshike na kutekeleza masharti haya.

13 “Mnapaswa kufanya Sherehe ya Vibanda*^g kwa siku saba mnapokusanya nafaka kutoka katika uwanja wenu wa kupuria na kutoka katika shinikizo lenu la mafuta na divai. **14** Shangilieni wakati wa sherehe yenu,^h ninyi na wana wenu, mabinti wenu, watumwa wenu wa kiume, vijakazi wenu, Walawi, wakaaji wage-ni, mayatima, na wajane walio ndani ya majiji yenu. **15** Kwa siku saba mtamfanyia Yehova Mungu wenu shereheⁱ mahali ambapo Yehova atachagua, kwa kuwa Yehova Mungu wenu atabariki mazao yenu yote na kila jambo mnalofa-

16:11 * Tnn., “malango.” 16:13, 16 * Au “Vibanda vya Muda.”

SURA YA 16

a Kut 12:16
Law 23:8

b Kut 23:16
Kut 34:22
Law 23:15

c Hes 28:26

d Kum 16:17
1Ko 16:2
2Ko 8:12

e Kum 12:5-7

f Kut 3:7
Kum 5:15

g Kut 23:16
Law 23:34
Hes 29:12
Kum 31:10, 11
Yoh 7:2

h Kum 12:12
Ne 8:10, 17
Mhu 5:18

i Law 23:36, 40
Ne 8:18

Safu ya 2

a Kum 7:13
Kum 28:8
Kum 30:16

b Flj 4:4
1Th 5:16

c Kut 23:14, 15

d Kum 16:10

e Kum 16:13

f 2Ko 8:12

g Kut 18:25, 26
Kum 1:16
2Nya 19:4, 5

h Kut 23:2
Law 19:15

i Kum 1:17

j Kut 23:8
1Sa 12:3
Mhu 7:7

k Mik 6:8

l Kut 34:13

m Kut 23:24
Law 26:1
Kum 12:3

SURA YA 17

n Law 22:20
Kum 15:21
Mal 1:8

nya,^a nanyi mtakuwa na shangwe kwelikweli.^b

16 “Mara tatu kwa mwaka, wanaume wenu wote wanapaswa kwenda mbele za Yehova Mungu wenu mahali atakapochagua: katika Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu,^c Sherehe ya Majuma,^d na Sherehe ya Vibanda,^{*e} na hakuna yeyote kati yao anayepaswa kwenda mbele za Yehova mikono mitupu. **17** Zawadi ambayo kila mtu ataleta inapaswa kulingana na baraka ambazo Yehova Mungu wenu amempa.^f

18 “Mnapaswa kuwaweka waamuzi^g na maofisa kwa ajili ya kila kabila katika majiji yenu yote ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, nao lazima wawahukumu watu kwa hukumu ya uadilifu. **19** Msipotoshe haki,^h msipendeele,ⁱ wala kukubali rushwa, kwa maana rushwa hupofusha macho ya wenye hekima^j na hupotosha maneno ya waadilifu. **20** Haki—mnapaswa kufuatia haki,^k ili mwendelee kuishi na kumiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa ninyi.

21 “Msipande mti wa aina yoyote na kuufanya kuwa mti mtakatifu*^l karibu na madhabahu ya Yehova Mungu wenu ambayo mtajitengeneza.

22 “Wala hampaswi kujisimamishia nguzo takatifu,^m kitu ambacho Yehova Mungu wenu anachukia.

17 “Usimtolee Yehova Mungu wako dhabihu ya ng’ombe dume au kondoo mwenye kasoro au mwenye tazitizo lolote, kwa sababu jambo hilo litakuwa chukizo kwa Yehova Mungu wako.ⁿ

16:21 * Angalia Kamusi, uku. 2012.

2 “Ikiwa mwanamume au mwanamke atapatikana miongoni mwenu, katika mojawapo ya majiji ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, aliyeye na mazoea ya kufanya uovu machoni pa Yehova Mungu wenu na kuvunja agano lake,^a 3 naye anapotoka na kuabudu miungu mingine na kuiinamia miungu hiyo au jua au mwezi au jeshi lote la mbinguni,^b jambo ambalo sijamuru,^c 4 ukiambiwa au kusikia habari hiyo, unapaswa kuchunguza jambo hilo kikamili. Ikithibitishwa ni kweli^d kwamba jambo hilo lenye kuchukiza limefanywa katika Israeli, 5 utamtoa nje ya malango ya jiji lenu mwanamume au mwanamke ambaye amefanya uovu huo, na lazima mwanamume au mwanamke huyo auawe kwa kupigwa mawe.^e 6 Kwa ushahidi wa* mashahidi wawili au watatu^f yule anayepaswa kufa atauawa. Hapaswi kuuawa kwa ushahidi wa shahidi mmoja.^g 7 Mikono ya mashahidi inapaswa kuwa ya kwanza kumuua, kisha mikono ya watu wengine wote. Ni lazima mwondoe uovu miongoni mwenu.^h

8 “Ikiwa kesi ambayo ni ngumu sana kwenu kumuua inatokea katika mojawapo ya majiji yenu, iwe ni kesi ya kuua*ⁱ au dai la kisheria limezushwa, au tendo la ukatili limefanywa, au mizozo mingine, mnapaswa kwenda mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua.^j 9 Nendeni kwa makuhani Walawi na kwa mwamuzi^k anayehudu-

17:6 *Tnn., “kinywa cha.” 17:8 *Tnn., “kumwaga damu.”

SURA YA 17

a Kum 4:23
Kum 13:6-9

b Kum 4:19

c Kum 13:12-15

d Yoh 7:51

e Kum 13:6, 10

f Mt 18:16
Yoh 8:17
1Ti 5:19
Ebr 10:28

g Hes 35:30
Kum 19:15

h Kum 13:5
1Ko 5:13

i Hes 35:11

j Kum 12:5
1Fa 3:16, 28
Zb 122:2, 5

k 1Sa 7:15, 16

Safu ya 2

a Kum 19:17
Kum 21:5

b Mal 2:7

c Kum 5:32
Kum 12:32

d Met 11:2
Ebr 10:28

e Kum 13:5
1Ko 5:13

f Kum 13:11
Kum 19:20

g 1Sa 8:5, 20
1Sa 10:19

h 1Sa 9:17
1Sa 10:24
1Sa 16:12, 13

i Kum 20:1
2Sa 8:4
Zb 20:7
Met 21:31

j Isa 31:1

k 1Fa 11:1-3
Ne 13:26

mu wakati huo, muwapelekee mashtaka yenu, nao watafanya uamuzi.^a 10 Kisha mnapaswa kutenda kulingana na uamuzi watakaofanya mahali hapo palipochaguliwa na Yehova. Muwe waangalifu kufanya mambo yote wanayo-waagiza. 11 Mnapaswa kutenda kulingana na sheria watakayowaonyesha na kulingana na uamuzi watakaowatangazia.^b Msigeuke na kucha uamuzi watakaofanya, na kwenda kulia au kushoto.^c 12 Mtu anayetenda kwa kimbelebele kwa kukataa kumsikiliza kuhani anayemhudumia Yehova Mungu wenu au kukataa kumsikiliza mwamuzi ni lazima afe.^d Ni lazima mwondoe uovu katika Israeli.^e 13 Basi watu wote watasikia na kuogopa, nao hawatatenda tena kwa kimbelebele.^f

14 “Mtakapoingia katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, mkaimiliki na kuishi humo, nanyi msemi, ‘Na tumweke mfalme juu yetu kama mataifa yote yanayotuzunguka,’^g 15 mnapaswa kumweka mfalme ambaye Yehova Mungu wenu atamchagua.^h Mnapaswa kumchagua mfalme kutoka miongoni mwa ndugu zenu. Hamruhusiwi kumweka mfalme ambaye ni mgeni, ambaye si ndugu yenu. 16 Hata hivyo, hapaswi kujipatia farasi wengiⁱ au kuwafanya watu warudi Misri kuchukua farasi wengi zaidi,^j kwa kuwa Yehova aliwaambia hivi: ‘Msirudi huko tena kamwe kupitia njia hii.’ 17 Wala hapaswi kuwa na wake wengi, ili moyo wake usipotoke;^k wala hapaswi kujipa-

tia fedha na dhahabu nyingi sana.^a **18** Atakapoketi kwenye kiti cha ufalme wake, ni lazima ajiandikie kwenye kitabu* nakala ya Sheria hii, kwa kutumia nakala inayowekwa na makuhani Walawi.^b

19 "Anapaswa kubaki nacho, naye lazima akisome sikuzote za maisha yake,^c ili aji-funze kumwogopa Yehova Mungu wake na kushika maneno yote ya Sheria hii na masharti haya kwa kuyatekeleza.^d **20** Hivyo moyo wake hautajikweza juu ya ndugu zake, naye hataacha amri hiyo na kwenda kulia au kushoto, ili aendelee kutawala kwa muda mrefu katika ufalme wake, yeye na wanawe katika Israeli.

18 "Makuhani Walawi, naam, kabila lote la Lawi, halitapewa fungu au urithi pamoja na Waisraeli. Watakula dhahabu zinazochomwa kwa moto zinazotolewa kwa Yehova, ambazo ni urithi wake.^e **2** Kwa hiyo hawapaswi kuwa na urithi kati ya ndugu zao. Yehova ndiye urithi wao, kama alivyowaambia.

3 "Sasa hii ndiyo haki ambayo makuhani wanastahili kutoka kwa watu: Mtu yeyote anayetoa dhahabu, iwe ni ng'ombe dume au kondoo anapaswa kumpa kuhani mguu wa mbele, mataya, na tumbo. **4** Mnapaswa kumpa mazao ya kwanza ya nafaka yenu, divai yenu mpya, mafuta yenu, na manyoya ya kwanza yaliyokatwa ya kondoo wenu.^f **5** Yehova Mungu wenu amewachagua wao pamoja na wanao kutoka kati ya makabila yenu yote ili

17:18 *Au "hati ya kukunjwa."

SURA YA 17

a Ayu 31:24, 28
1Ti 6:9

b Kum 31:9, 26
2Fa 22:8

c 2Nya 34:18

d Zb 1:2
Zb 119:97

SURA YA 18

e Hes 18:20, 24
Kum 10:9
Yos 13:14, 33
1Ko 9:13

f Kut 23:19
Hes 18:8, 12
2Nya 31:4
Ne 12:44

Safu ya 2

a Kut 28:1
Hes 3:10
Kum 10:8

b Hes 35:2

c Kum 12:5, 6
Kum 16:2
Zb 26:8

d 2Nya 31:2

e Law 7:10

f Law 18:26
Kum 12:30

g Kum 12:31
2Fa 16:1, 3
2Nya 28:1, 3
Zb 106:35-37
Yer 32:35

h 2Fa 17:17
Mdo 16:16

i Law 19:26
Mdo 19:19

j Eze 21:21

k Kut 22:18

l Law 20:27
1Nya 10:13

m Law 19:31

n 1Sa 28:7-11
Isa 8:19
Gal 5:19, 20

o Mt 5:48
2Pe 3:14

wahudumu katika jina la Yehova daima.^a

6 "Lakini ikiwa Mlawi ataoondoka katika mojawapo ya majiji yenu katika Israeli alimokuwa akiishi,^b naye angependa kwenda mahali ambapo Yehova anachagua,^{*c} **7** anaweza kuhudumu huko katika jina la Yehova Mungu wake kama wanavyofanya ndugu zake wote, Walawi, wanaosimama huko mbele za Yehova.^d

8 Atapokea kiasi kilekile cha chakula pamoja nao,^e mbali na malipo anayopata baada ya kuuzwa mali za mababu zake.

9 "Mtakapoingia katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, msijifunze kuiga mazoea yenye kuchukiza ya mataifa hayo.^f **10** Asipatikane miongoni mweni mtu yeyote anayemtekeza* motoni^g mwanawe au binti yake, mtu yeyote anayefanya uaguzi,^{#h} mtu yeyote anayefanya uchwawi,ⁱ mtu yeyote anayetafuta ishara za ubashiri,^j mlozi,^k **11** mtu yeyote anayefwanga wenzake kwa uchawi, mtu yeyote anayetafuta ushauri kutoka kwa watu wanaowasiliana na roho,^l mpiga ramli,^m au mtu yeyote anayetafuta habari kuhusu wafu.ⁿ **12** Kwa maana mtu yeyote anayefanya mambo haya ni chukizo kwa Yehova, na kwa sababu ya mazoea haya yanayochukiza, Yehova Mungu wenu anayafukuza mataifa hayo kutoka mbele yenu. **13** Mnapaswa kudhihirisha kwamba hamna lawama mbele za Yehova Mungu wenu.^o

18:6 *Yaani, mahali ambapo Yehova anachagua kuwa kitovu cha ibada. **18:10** *Tnn., "anayempitisha." #Au "anayebashiri."

14 “Kwa maana mataifa haya mnyomiliki nchi yao yalikuwa yakiwasikiliza wale waliozoea uchawi^a na uaguzi,^{*b} lakini Yehova Mungu wenu hawajawaruhusu mfanye jambo lolote kama hilo. **15** Yehova Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka kati ya ndugu zenu. Ni lazima mumsikilize.^c **16** Kwa sababu hilo ndilo mlilomwomba Yehova Mungu wenu kule Horebu katika siku ya kusanyiko,^{*d} mliposema, ‘Usiache tusikie sauti ya Yehova Mungu wetu au kuona tena moto huu mkubwa, tusije tukafa.’^e **17** Kisha Yehova akaniambia, ‘Jambo walilosema ni sawa. **18** Nitawainulia nabii^f kama wewe kutoka kati ya ndugu zao, nami nitaweka maneno yangu katika kinyua chake,^g naye atawaambia mambo yote nitakayomwamuru.’^h **19** Naam, nitamwadhibu kila mtu ambaye hatasikiliza maneno yangu ambayo nabii huyo atasema katika jina langu.’ⁱ

20 “Ikiwa nabii yeyote atasema kwa kimbelembele katika jina langu neno ambalo sikumwamuru asema au kusema katika jina la miungu mingine, nabii huyo lazima afe. **21** Lakini huenda mkasema hivi mioyoni mwenu: “Tutajuaaje Yehova hajasema neno hilo?” **22** Nabii akisema neno katika jina la Yehova na neno hilo lisitimie au kufanyika, basi Yehova hakusema neno hilo. Nabii huyo alilisema kwa kimbelembele. Hampaswi kumwogopa.’

18:14 *Au “ubashiri.” 18:16 *Au “kukutanika.”

SURA YA 18

a Law 19:26
2Fa 21:1, 2, 6

b Yos 13:22

c Mwa 49:10
Hes 24:17
Lu 7:16
Yoh 1:45
Yoh 6:14
Mdo 3:22
Mdo 7:37

d Kut 19:17

e Kut 20:19

f Kut 34:28
Hes 12:3
Mt 4:1, 2
Mt 11:29
Yoh 5:46

g Yoh 17:8

h Yoh 12:49
Ebr 1:2

i Mdo 3:23

j Kum 13:1-5
Yer 28:11-17

Safu ya 2

SURA YA 19

a Kum 7:1
Kum 9:1

b Hes 35:14
Yos 20:7, 9

c Hes 35:15
Kum 4:42

d Hes 35:25

e Hes 35:12, 19

f Yos 20:4, 5

g Mwa 15:18
Kut 23:31
Kum 11:24

h Mwa 28:14

19 “Yehova Mungu wenu atakapoyaangamiza mataifa ambayo Yehova Mungu wenu anawapa nchi yao na mtakapokuwa mmemiliki nchi yao na kuishi katika majiji yao na nyumba zao,^a **2** mnapaswa kutenga majiji matatu katikati ya nchi yenu ambayo Yehova Mungu wenu anawapa mwimiliki.^b **3** Mnapaswa kugawanya mara tatu eneo la nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa mwimiliki, nanyi mtengeneze barabara ili muuaji yeyote aweze kukimbilia katika mojawapo ya majiji hayo.

4 “Sasa hivi ndivyo itakavyokuwa kuhusu muuaji ambaye huenda akakimbilia humo ili kuokoa uhai wake: Akimuaa jirani yake bila kukuudia naye hakuwa akimchukia;^c **5** kwa mfano, anapoeenda na jirani yake msituni kukusanya kuni, kisha anainua mkono wake ili akate mti kwa shoka, lakini shoka lichomoke kwenye mpini na kumgonga jirani yake na kumuua, muuaji huyo anapaswa kukimbilia katika mojawapo ya majiji hayo.^d **6** Asipofanya hivyo, mtu anayelipiza kisasi cha damu^e anaweza kwa hasira kali kumkimbiza, kumkamata, na kumuua, kwa sababu jiji hilo lilikuwa mbali sana. Hata hivyo, hakustahili kufa kwa sababu hakuwa akimchukia jirani yake.^f **7** Ndiyo sababu ninawaamuru hivi: ‘Tengeni majiji matatu.’

8 “Yehova Mungu wenu akipanua eneo lenu kama alivyowaapia mababu zenu^g na kuwapa nchi yote aliyohidi kuwapa mababu zenu^h **9** —maadamu mnashika kwa

uaminifu amri hii yote ninayowapa leo, kwa kumpenda Yehova Mungu wenu na kutebebea daima katika njia zake^a—basi mtaongeza majiji mengine matatu zaidi ya hayo matatu.^b **10** Hivyo hakuna damu isiyo na hatia itakayomwagwa^c katika nchi yenu ambayo Yehova Mungu wenu anawapa kuwa urithi, nanyi hamtakuwa na hatia yoyote ya damu.^d

11 “Lakini ikiwa mtu alikuwa akimchukia jirani yake,^e akamvizia, akamjeruhi vibaya sana na kumuua, na mtu huyo amekimbilia katika mojawapo ya majiji hayo, **12** basi wazee wa jiji lake wanapaswa kumwita kutoka humo na kumtia mikononi mwa yule anayelipiza kisasi cha damu, naye lazima afe.^f **13** Hampaswi kumhurumia,^{*} nanyi lazima mwondoe hatia ya damu isiyo na hatia kutoka katika Israeli,^g ili mambo yawaendee vyema.

14 “Mtakapopokea urithi wenu katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa mwimiliki, hampaswi kusogezwa alama ya mpaka^h wa jirani yenu kutoka mahali ambapo uliwekwa na mababu zenu.

15 “Shahidi mmoja hawezi kufanya mtu mwingine ahukumiwe kwa kosa lolote au dhambi yoyote ambayo huenda ametenda.ⁱ Jambo hilo linapaswa kuthibitishwa kwa ushahidi wa^{*} mashahidi wawili au mashahidi watatu.^j **16** Shahidi mwenye nia ya kumdheru mwingine akitoa ushahidi dhidi ya mtu na kumshtaki kwa kosa fulani,^k **17** watu hao wawili wanaozozana wa-

19:13 * Tnn., “Jicho lenu lisimhurumie.”
19:15 * Tnn., “kinywa cha.”

SURA YA 19

a Kum 11:22, 23

b Yos 20:7, 8

c Met 6:16, 17

d Kum 21:6-9

e 1Yo 3:15

f Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:16
Kum 27:24g Law 24:17, 21
Hes 35:33
2Sa 21:1

h Kum 27:17

i Hes 35:30
Kum 17:6j Mt 18:16
Yoh 8:17
2Ko 13:1
1Ti 5:19k Kut 23:1
1Fa 21:13
Mk 14:56

Safu ya 2

a Kum 17:8, 9

b Kum 13:14
Kum 17:4
2Nya 19:6

c Met 19:5

d Kum 21:20, 21
Kum 24:7
1Ko 5:13e Kum 13:11
Kum 17:13
1Ti 5:20

f Kum 19:13

g Kut 21:23-25
Mt 5:38

SURA YA 20

h Kum 3:22
Kum 31:6
Zb 20:7
Met 21:31

i Hes 31:6

j Kut 14:14
Yos 23:10

tasimama mbele za Yehova, mbele ya makuhani na waa-muzi watakaokuwa wakihudumu wakati huo.^a **18** Waamuzi watachunguza jambo hilo kikamili,^b na ikiwa mtu huyo ni shahidi wa uwongo na amelea shtaka la uwongo dhidi ya ndugu yake, **19** mnapaswa kumtenda kama alivyopanga kumtendea ndugu yake kwa hila,^c nanyi lazima mwondoe uovu miongoni mwenu.^d **20** Wale wanaobaki wata-sikia na kuogopa, nao hawatatenda tena kamwe uovu kama huo miongoni mwenu.^e **21** Hampaswi^{*} kuwahurumia:^f Uhai utatolewa kwa uhai,^g jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu.^g

20 “Mkienda vitani kupigana na na maadui wenu na kuona kwamba farasi wao na magari yao ya vita na wanajeshi wao ni wengi kuliko ninyi, msiwaogope, kwa maana Yehova Mungu wenu aliye-watoa nchini Misri yuko pamoja nanyi.^h **2** Mnapokaribia kwenda vitani, kuhani anapaswa kuja na kuwahutubia watu.ⁱ **3** Anapaswa kuwaambia hivi: ‘Sikilizeni, enyi Waisraeli, hivi punde mtapigana na maadui wenu. Msife moyo. Msiogope wala msihofu wala kutetemeka kwa sababu yao, **4** kwa maana Yehova Mungu wenu anapiga-nie dhidi ya maadui wenu na kuwaokoa ninyi.’^j

5 “Maofisa pia wanapaswa kuwaambia watu hivi: ‘Ni nani ambaye amejenga nyumba mpya lakini hajaizindua?

19:21 * Tnn., “Jicho lenu halipaswi.”
* Tnn., “Nafsi itatolewa kwa nafsi.”

Na arudi nyumbani kwake. La sivyo, huenda akauawa vitani na mwanamume mwingine aizindue. **6** Na ni nani ambaye amepanda shamba la mizabibu na hajaanza kuvuna matunda yake? Na arudi nyumbani kwake. La sivyo, huenda akauawa vitani na mwanamume mwingine akaanza kuvuna matunda yake. **7** Na ni nani ambaye amemchumbia mwanamume lakini hajamwoa? Na arudi nyumbani kwake.^a La sivyo, huenda akauawa vitani na mwanamume mwingine amwoe.^b **8** Maofisa hao wanapaswa pia kuwauliza watu, ‘Ni nani anayeogopa na aliye na moyo dhaifu?’^b Anapaswa kurudi nyumbani kwake, ili asiwafanye ndugu zake wawunjike moyo kama yeye.^{*c} **9** Baada ya maofisa hao kuzungumza na watu, wanapaswa kuwaweka wakuu wa majeshi ili wawaongoze watu.

10 “Mnapokaribia jiji ili kupigana nalo, mnapaswa kulingangazia pia masharti ya amani.^d **11** Jiji hilo likikubali kufanya amani pamoja nanyi na kuwafungulia malango yake, watu wote waliomo humo watakuwa wafanyakazi wenu wa kazi za kulazimishwa, nao watawatumikia.^e **12** Lakini likikataa kufanya amani pamoja nanyi na kupigana nanyi, mnapaswa kulizingira, **13** na kwa hakika Yehova Mungu wenu atalitia mikononi mwenu, nanyi mtamuua kwa upanga kila mwanamume aliye ndani ya jiji hilo. **14** Hata hivyo, mtajichukulia wanawake, watoto, mifugo, na kila

20:8 *Au “asifanye mioyo ya ndugu zake iyeyuke kama moyo wake mwenyewe.”

SURA YA 20

a Kum 24:5

b Amu 7:3

c Hes 13:33
Hes 14:1-3
Hes 32:9
Kum 1:28

d Yos 11:19

e Law 25:44, 46
Yos 9:22, 27

Safu ya 2

a 2Nya 14:13

b Yos 22:8

c Yos 6:17
Yos 10:28
Yos 11:11

d Kum 7:1

e Kut 34:15
Kum 7:4
Yos 23:12, 13
Isa 2:6
IKo 5:6
IKo 15:33

f Ne 9:25

SURA YA 21

g Kum 16:18

kitu kilicho jijini, nyara zake zote,^a nanyi mtakula nyara za maadui wenu ambazo Yehova Mungu wenu amewapa ninyi.^b

15 “Hivyo ndivyo mtakavyoyatendea majiji yote yaliyo mbali sana nanyi ambayo si majiji ya mataifa haya yaliyo karibu. **16** Lakini katika majiji ya mataifa haya, ambayo Yehova Mungu wenu anawapa yawe urithi wenu, hampaswi kuacha hai kitu chocho te kinachopumua.^c **17** Mnapaswa kuwaangamiza kabisa, Wahiti, Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi,^d kama Yehova Mungu wenu alivyowaamuru; **18** ili wasiwafundishe kufuata mazoea yao yote yenye kuchukiza wanayofanya miungu yao, na hivyo kuwafanya mumtendee dhambi Yehova Mungu wenu.^e

19 “Mkilizingira jiji ili kuli-teka na mmekuwa mkipigana nalo kwa siku nyingi, hampaswi kuharibu miti yake kwa kuikata ovyoovyo kwa shoka. Mnaweza kula matunda yake, lakini hampaswi kuikata.^f Je, mnapaswa kuushambulia mti kama mnavyomshambulia mwanadamu? **20** Mnaweza kuharibu tu mti ambao mnajua hautumiwi kwa chakula. Mnaweza kuukata na kuutumia kulizingira jiji linalopigana nanyi, mpaka litakapoa nguka.

21 “Mtu akipatikana ameuawa uwanjani katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa mwimiliki na haijulikani ni nani aliyemuua, **2** wazee na waamuzi^g wenu wanapaswa kwenda na kupima umbali kutoka kwenye maiti hiyo mpaka kwenye majiji yaliyo karibu nayo. **3** Kisha wazee wa jiji lililo karibu

na maiti hiyo wanapaswa kuchukua kutoka kati ya mifugo ng'ombe mchanga ambaye hajawahi kutumiwa kufanya kazi, ambaye hajawahi kuvuta nira, **4** na wazee wa jiji hilo watampeleka ng'ombe huyo mchanga kwenye bonde* linalotiririka maji ambalo halijalimwa wala kupandwa mbe-gu, nao wanapaswa kumvunja shingo ng'ombe huyo mchanga humo bondeni.^a

5 "Nao makuhani, Walawi, watakuja kwa sababu Yehova Mungu wenu amewachagua wamhudumie,^b watangaze baraka katika jina la Yehova.^c Watatangaza jinsi kila mzozo unaohusisha ukatili unavyopaswa kusuluhishwa.^d **6** Kisha wazee wote wa jiji lililo karibu zaidi na maiti hiyo wanapaswa kunawa mikono yao^e juu ya ng'ombe huyo mchanga ambaye alivunja shingo bondeni, **7** nao wanapaswa kutangaza hivi: 'Mikono yetu haikumwaga damu hii, wala macho yetu hayakuona iki-mwagwa. **8** Usiwahesabie hatia hiyo watu wako Waisraeli, ambao uliwakombo, ^f Ee Yehova, nawe usiache hatia ya damu isiyo na lawama ibaki miongoni mwa watu wako Waisraeli.'^g Nao hawatakuwa na hatia hiyo ya damu. **9** Kwa njia hiyo mtaondoa hatia ya damu isiyo na lawama kutoka miongoni mwenu kwa kufanya yaliyo sawa machoni pa Yehova.

10 "Mkienda vitani kupigana na maadui wenu na Yehova Mungu wenu awasaidie kuwashinda, nanyi mwachukue mateka,^h **11** ukiona mwanamke mrembo miongoni mwa ma-

SURA YA 21

a Hes 35:33

b Kut 28:1

c Hes 6:23-27
1Nya 23:13

d Kum 17:8, 9

e Zb 26:6
Mt 27:24

f 2Sa 7:23

g Isa 26:21
Yer 26:15h Hes 31:9
Kum 20:13, 14

Safu ya 2

a Hes 20:29
Kum 34:8

b Kum 24:1

c Mwa 29:30, 33

d Mwa 25:31
2Nya 21:3

teka hao na kuvutiwa naye, nawe utake kumchukua awe mke wako, **12** unaweza kumleta nyumbani mwako. Kisha atanyoa kichwa chake, atatunza kucha zake, **13** na kuvua nguo alizokuwa amevaa alipotekwa, naye ataishi nyumbani mwako. Atamlilia baba yake na mama yake kwa mwezi mzima,^a kisha unaweza kulala naye; utakuwa mume wake naye atakuwa mke wako. **14** Lakini ikiwa hupe-ndezwi naye, unapaswa kumruhusu aende zake^b mahali popote anapotaka. Lakini huwezi kumuza upate pesa au kumtesa, kwa kuwa umemwai-bisha.

15 "Ikiwa mwanamume ana wake wawili, naye anampenda mmoja zaidi ya mwenzake* na wote wawili wame-mzalia wana na mzaliwa wa kwanza ni wa mwanamke asiyependwa sana,^c **16** siku atakapowapa wanawe urithi wake, hataruhusiwa kumten-dea mwana wa mwanamke anayependwa kana kwamba ndiye mzaliwa wake wa kwanza na kumpuza mwana wa mwanamke asiyependwa sana, ambaye ndiye mzaliwa wa kwanza. **17** Anapaswa kumtambua mwana wa mwanamke asiyependwa sana kwa mzaliwa wa kwanza kwa kumpa maradufu ya kila kitu alichu nacho, kwa sababu mwana huyo ndiye mwanzo wa nguvi zake za uzazi. Haki ya mzaliwa wa kwanza ni yake.^d

18 "Ikiwa mtu ana mwana ambaye ni mkaidi na mwasi na hamtii baba yake au mama

21:15 * Tnn., "wake wawili, mmoja anayependwa na mwengine anayechukiwa."

yake,^a nao wamejaribu kumre-
kebisha lakini anakataa ku-
wasikiliza,^b **19** baba yake
na mama yake wanapaswa ku-
mshika na kumpeleka kwa wa-
zee kwenye lango la jiji lake
20 na kuwaambia hivi wa-
zee wa jiji lake: ‘Huyu mwa-
na wetu ni mkaidi na mwasi,
anakataa kututii. Ni mlafi^c na
mlevi.’^d **21** Basi watu wote
wa jiji lake watamua kwa ku-
mpiga mawe. Kwa hiyo ni la-
zima mwondoe uovu miongo-
ni mwenu, na Waisraeli wote
watasikia na kuogopa.^e

22 “Mtu akitenda dhambi
inayostahili hukumu ya kifo,
naye ameuawa,^f na mmentu-
ndika mtini,^g **23** maiti yake
isibaki mtini usiku kucha.^h Ba-
dala yake, mnapaswa kuhaki-
kisha kwamba mnaizika siku
hiyohiyo, kwa sababu mtu ali-
yitundika na kitu kilicholaa-
niwa na Mungu,ⁱ nanyi hampa-
swi kuichafua nchi ambayo
Yehova Mungu wenu anawapa
iwe urithi wenu.^j

22 “Ukimwona ng’ombe
dume wa ndugu yako
au kondoo wake akipotea njia,
usimpuuze kimakusudi.^k Unap-
aswa kumrudisha kwa ndu-
gu yako. **2** Lakini ikiwa
huyo ndugu yako haishi ka-
ribu nawe au humjui, unapa-
swa kumpeleka mnyama huyo
nyumbani kwako, naye ata-
kaa nawe mpaka ndugu yako
atakapokuja kumtafuta. Kisha
utamrudishia mnyama huyo.^l
3 Unapaswa kufanya vivyo hi-
vyo kuhusu punda wake, nguo
zake, na kitu chochote uta-
kachopata kilichopotezwa na
ndugu yako. Hupaswi kuki-
puza.

4 “Ukimwona punda wa
ndugu yako au ng’ombe dume

SURA YA 21

a Kut 20:12
Kum 27:16
Met 1:8
Efe 6:1

b Kum 8:5
Met 13:24
Met 19:18
Met 23:13
Ebr 12:9

c Met 28:7

d Ro 13:13
1Ko 6:10
Efe 5:18

e Kum 13:10, 11

f Hes 25:5

g Yos 10:26
Mdo 10:39

h Yos 8:29
Yoh 19:31

i Gal 3:13

j Hes 35:34

SURA YA 22

k Kut 23:4

l Mt 7:12

Safu ya 2

a Kut 23:5
Law 19:18
Lu 10:27
Gal 6:10

b Law 22:28
Zb 145:9
Met 12:10
Mt 10:29

c 2Sa 11:2
Mdo 10:9

d Law 19:19

e Met 12:10

f Law 19:19

g Hes 15:38
Mt 23:2, 5

wake akianguka barabarani
hupaswi kumpuuza kimaku-
sudi. Unapaswa kumsaidia ku-
mwinua mnyama huyo.^a

5 “Mwanamke hapaswi ku-
vaa nguo za mwanamume, na
mwanamume hapaswi kuvaa
nguo za mwanamke. Kwa maa-
na mtu yeyote anayefanya hi-
vyo ni chukizo kwa Yehova
Mungu wenu.

6 “Ukipata njiani kiota cha
ndege chenye makinda au ma-
yai, iwe mtini au kwenye
ardhi, naye mama amefuni-
ka makinda au kuatamia ma-
yai, usimchukue mama pamo-
ja na makinda yake.^b **7** Ha-
kikisha umemfukuzwa mama
yao, lakini unaweza kuchukua
makinda. Fanya hivyo ili ma-
mbo yakuendee vyema na ui-
shi muda mrefu.

8 “Ukijenga nyumba mpya,
ni lazima pia ujenege ukuta ku-
zunguka ukingo wa paa lako,^c
ili mtu asianguke kutoka kwe-
nye paa nawe uiletee familia
yako hatia ya damu.

9 “Usipande aina mbili za
mbegu katika shamba lako la
mizabibu.^d La sivyo, mazao
yote utakayopata kutokana na
mbegu hizo na pia zabibu zi-
takuwa za mahali patakatifu.

10 “Usilime kwa ng’ombe
dume na punda pamoja.^e

11 “Usivae nguo zilizote-
ngenezwa kwa kuchanganya
sufu na kitani.^f

12 “Unapaswa kutengeneza
vishada kwenye pembe nne za
nguo unazovaa.^g

13 “Mwanamume akimchu-
kua mke na kufanya ngono
naye lakini baadaye amchu-
kie* **14** na kudai kwamba
ana mwenendo mbaya na

22:13 *Au “amkatae.”

kumharibia sifa kwa kusema, 'Nilimchukua mwanamke huyu, lakini nilipofanya ngono naye sikupata uthibitisho wa kwamba yeye ni bikira,' **15** baba na mama ya msichana huyo wanapaswa kuwapelekea wazee walio kwenye lango la jiji uthibitisho wa kwamba msichana huyo alikuwa bikira. **16** Baba ya msichana huyo atawaambia hivi wazee hao: 'Nilimpa mwanamume huyu binti yangu awe mke wake, lakini anamchukia* **17** na anadai kwamba ana mwenendo mbaya kwa kusema, "Nimegundua kwamba binti yenu si bikira." Sasa huu ndio uthibitisho wa ubikira wa binti yangu.' Kisha watatandaza nguo hiyo mbele ya wazee wa jiji. **18** Wazee wa jiji^a watamchukua mwanamume huyo na kumtia nidhamu.^b **19** Watamtoza shekeli 100 za fedha na kumpa baba ya msichana huyo, kwa sababu mtu huyo alimharibia sifa bikira wa Israeli,^c naye atae ndelea kuwa mke wake. Maudamu mwanamume huyo anishi, hataruhusiwa kumtaliki msichana huyo.

20 "Hata hivyo, ikiwa madai hayo ni ya kweli na hakuna uthibitisho kwamba msichana huyo alikuwa bikira, **21** wanapaswa kumpeleka msichana huyo kwenye mlango wa nyumba ya baba yake, na wanaume wa jiji watamua kwa kumpiga mawe, kwa sababu ametenda jambo la aibu^d katika Israeli kwa kufanya uasherati* katika nyumba ya baba yake.^e Kwa hiyo ni lazi-

22:16 *Au "anamkataa." 22:21 *Au "ukahaba."

SURA YA 22

a Kut 18:21
Kum 1:13
Kum 16:18

b Kum 25:2
Met 10:13
Met 19:29

c Mal 2:16

d Ebr 13:4

e Law 21:9

Safu ya 2

a Law 11:45
1Ko 5:13

b Mwa 20:3
Kut 20:14
Law 20:10
1Ko 6:9,10
1Ko 6:18

c Law 20:10
Kum 5:18
1Th 4:3, 6
Ebr 13:4

d Mwa 4:8
Hes 35:20, 21
Yak 2:11

e Mwa 34:2, 5

ma mwondoe uovu miongoni mwenu.^a

22 "Mwanamume akipatikana akifanya ngono na mke wa mwanamume mwingine, ni lazima wote wawili wauawe pamoja, mwanamume huyo pamoja na mwanamke aliyefanya naye ngono.^b Kwa hiyo ni lazima mwondoe uovu katika Israeli.

23 "Ikiwa bikira amechumbiwa na mwanamume, kisha mwanamume mwingine akutane naye jijini na kufanya naye ngono, **24** mnapaswa kuwaleta wote wawili kwenye lango la jiji na kuwaua kwa kuwapiga mawe, mtamua msichana huyo kwa sababu hakupiga mayowe jijini na mwanamume huyo kwa sababu alimwaibisha mke wa mwanamume mwenzake.^c Kwa hiyo ni lazima mwondoe uovu miongoni mwenu.

25 "Hata hivyo, ikiwa mwanamume huyo alimkuta uwanjani msichana huyo aliyechumbiwa na kumkamata kwa nguvu na kufanya naye ngono, mwanamume huyo aliyelala naye atauawa peke yake, **26** lakini msimtendee lolote msichana huyo. Msichana huyo hatatenda dhambi inayostahili kifo. Kisa chake ni sawa na cha mtu anayemshambulia mwenzake na kumuua.^d **27** Kwa maana mwanamume huyo alimkuta uwanjani, na msichana huyo aliyechumbiwa akapiga mayowe, lakini hakukuwa na mtu wa kumwoko.

28 "Mwanamume akikutana na bikira ambaye hajachumbiwa kisha amkamate kwa nguvu na kufanya naye ngono, nao wagunduliwe,^e **29** mwanamume aliyefanya ngono na

msichana huyo anapaswa kumpa baba ya msichana huyo shekeli 50 za fedha, naye atakuwa mke wake.^a Kwa sababu mwanamume huyo alimwaibisha, hataruhusiwa kumtaliki msichana huyo maisha yake yote.

30 “Hakuna mwanamume anayepaswa kumwoa* mke wa baba yake, ili asimwaibishe baba yake.”^b

23 “Mwanamume yeyote aliyehasiwa kwa kuminywa mapumbu au kwa kukatwa uume wake hapaswi kuja katika kutaniko la Yehova.^c

2 “Hakuna mwanaharamu anayepaswa kuingia katika kutaniko la Yehova.^d Hata kufikia kizazi cha kumi, hakuna mzao wake yeyote anayepaswa kuja katika kutaniko la Yehova.

3 “Hakuna Mwamoni au Mmoabu anayepaswa kuja katika kutaniko la Yehova.^e Hata kufikia kizazi cha kumi, hakuna mzao wao yeyote anayepaswa kuja katika kutaniko la Yehova, **4** kwa sababu hawakuwasaidia kwa kuwapa chakula na maji mlipokuwa njiani kutoka Misri,^f na kwa sababu walimkodi Balaamu mwana wa Beori kutoka Pethori kule Mesopotamia ili awalaani ninyi.^g **5** Lakini Yehova Mungu wenu alikataa kumsikiliza Balaamu.^h Badala yake, Yehova Mungu wenu alibadili laana hiyo ikawa baraka kwenu,ⁱ kwa sababu Yehova Mungu wenu aliwapenda.^j **6** Hapaswi kamwe kuhangaikia hali yao wala kuwasaidia kupata ufanisi siku zenu zote.”^k

22:30 *Tnn., “kumchukua.” #Tnn., “asimfunue nguo baba yake.”

SURA YA 22

a Mwa 34:11, 12
Kut 22:16

b Law 18:8
Law 20:11
Kum 27:20
IKo 5:1

SURA YA 23

c Law 21:18, 20
Isa 56:4, 5

d Kut 20:14
Law 20:10

e Ne 13:1, 2

f Amu 11:18

g Hes 22:6
Yos 24:9

h Hes 22:35

i Hes 23:11, 25
Hes 24:10

j Kum 7:7, 8

k 2Sa 8:2
2Sa 12:31

Safu ya 2

a Mwa 25:25, 26
Mwa 36:1
Hes 20:14

b Mwa 46:6
Law 19:34
Zb 105:23

c 1Sa 21:5
2Sa 11:11

d Law 15:16

e Law 15:31

f Law 26:12

g 1Pe 1:16

h Kut 22:21

7 “Msimchukie Mwedomu, kwa sababu yeye ni ndugu yenu.^a

“Msimchukie Mmisri, kwa maana mlikuwa wakaaji wage-ni katika nchi yao.^b **8** Kizazi cha tatu cha watoto wao kina-weza kuja katika kutaniko la Yehova.

9 “Mnapopiga kambi ili kuwashambulia maadui wenu, mnapaswa kuepuka kitu chochote kibaya.*^c **10** Ikiwa mwanamume ni mchafu kwa sababu ametokwa na shahawa usiku,^d anapaswa kwenda nje ya kambi, asirudi kambini. **11** Ifikapo jioni, anapaswa kuoga kwa maji, kisha anaweza kurudi kambini jua linapotua.^e **12** Mahali pa faragha* panapaswa kutengwa nje ya kambi, na mnapaswa kwenda kujisaidia huko. **13** Kati ya vifaa vyenu mtakuwa na kijiti. Mnapochuchumaa nje, mnapaswa kukitumia kuchimba shimo na kisha kufunika kinyesi chenu. **14** Kwa maana Yehova Mungu wenu anatembea katika kambi yenu^f ili awakomboe na kuwatia maadui wenu mikononi mwenu, na lazima kambi yenu iwe takatifu,^g ili asione kitu chochote kichafu ndani yenu, naye ageuke na kuacha kutembea pamoja nanyi.

15 “Mtumwa akimkimbia bwana wake na kuja kwako usimrudishe kwa bwana wake. **16** Anaweza kukaa pamoja nawe mahali popote atakapochagua katika mojawapo ya majiji yenu, popote anapopenda. Usimtese.^h

17 “Binti yeyote wa Israeli hapaswi kuwa kahaba wa he-

23:9 *Au “kinachochafua.” 23:12 *Yaani, choo.

kaluni,^a wala mwana yeyote wa Israeli hapaswi kuwa khaba wa hekaluni.^b **18** Hampaswi kuleta mapato ya mwanamke kahaba au mapato* ya mwanamume khaba[#] katika nyumba ya Yehova Mungu wenu ili kutimiza nadhiri, kwa sababu vyote vilivili ni chukizo kwa Yehova Mungu wenu.

19 “Usimtoze riba ndugu yako,^c iwe ni riba ya mkopo wa pesa, chakula, au kitu chochote kinachoweza kutozwa riba. **20** Unaweza kumtoza riba mgeni,^d lakini usimtoze riba ndugu yako,^e ili Yehova Mungu wako akubariki katika kazi zote utakazofanya katika nchi mnayoenda kumiliki.^f

21 “Ukiweka nadhiri kwa Yehova Mungu wako,^g usikawie kuitimiza.^h Kwa maana Yehova Mungu wako kwa hakika atakudai; la sivyo, utakuwa umetenda dhambi.ⁱ **22** Lakini usipoweka nadhiri, hutakuwa na hatia ya dhambi.^j **23** Unapaswa kutimiza maneno ya kinywa chako,^k na ni lazima utekeleze nadhiri uliyoweka kwa kinywa chako mwenyewe kama toleo la hiari kwa Yehova Mungu wako.^l

24 “Ukiingia katika shamba la mizabibu la jirani yako, unaweza kula zabibu za kutosha mpaka utosheke, lakini hupaswi kutia zabibu zozote katika chombo chako.^m

25 “Ukiingia katika shamba la nafaka la jirani yako, unaweza kukwanyua kwa mkono wako masuke yaliyokomaa, lakini hupaswi kutumia mundu kukata nafaka ya jirani yako.ⁿ

23:18 *Au “malipo.” Tnn., “bei.” #Tnn., “mbwa.”

SURA YA 23

a Law 19:29
Law 21:9

b 1Fa 14:24
2Fa 23:7

c Kut 22:25
Law 25:36, 37
Ne 5:10
Zb 15:5

d Kum 15:6

e Met 28:8

f Kum 15:4
Kum 15:7, 10
Met 19:17
Lu 6:34, 35

g Amu 11:30, 31
1Sa 1:11

h Yon 2:9

i Mhu 5:4, 6

j Mhu 5:5

k Hes 30:2
Zb 15:4
Met 20:25

l Amu 11:35
1Sa 14:24
Mt 5:33

m Mt 6:11
Ro 13:10

n Mt 12:1
Lu 6:1

Safu ya 2

SURA YA 24

a Mt 5:31, 32
Mk 10:4, 11

b Mal 2:16
Mt 1:19
Mt 19:3-8

c Law 21:7

d Kum 20:7
Met 5:18
Mhu 9:9

e Kut 22:26, 27

f Mwa 37:28
Mwa 40:15

g Kut 21:16

24 “Mwanamume akimwoa mwanamke lakini hapeandezwi naye kwa sababu ameona jambo fulani lisilofaa kwake, ni lazima amwandikie mwanamke huyo cheti cha talaka,^a ampe, na kumruhusu aondoke nyumbani mwake.^b **2** Akiondoka katika nyumba hiyo, anaweza kwenda kuolewa na mwanamume mwingine.^c **3** Mwanamume huyo wa pili akimchukia* na kumwandikia cheti cha talaka, kisha ampe na kumruhusu aondoke nyumbani mwake, au mwanamume huyo wa pili aliyemwoa akifa, **4** mume wake wa kwanza aliyemfukuza hataruhusiwa kumchukua tena awe mke wake baada ya mwanamke huyo kutiwa unajisi, kwa maana jambo hilo ni chukizo kwa Yehova. Hampaswi kuleta dhambi katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anapawa kuwa urithi.

5 “Mwanamume aliyepaswa karibuni hapaswi kutumikia jeshini wala kupewa majukumu mengine yoyote. Anapaswa kuwa huru kwa mwaka mmoja na kubaki nyumbani ili amfurahishe mke wake.^d

6 “Hakuna mtu anayepaswa kuchukua jiwe la chini la kusagia au jiwe la juu kuwa dhamana kwa ajili ya mkopo,^e kwa sababu kufanya hivyo ni sawa na kuchukua riziki ya[#] mtu kuwa dhamana.

7 “Ikiwa mtu atapatikana akiwa amemteka nyara ndugu yake Mwisraeli, naye amemtesa na kumuuzi, f mteka ji nyara huyo lazima auawe.^g

24:3 *Au “akimkataa.” 24:6 *Au “rehani.” #Au “kuchukua uhai wa; kuchukua nafsi ya.”

Mnapaswa kuondoa uovu miongoni mwenu.^a

8 “Ikiwa ugonjwa wa ukoma* umetokea na kuenea, muwe waangalifu sana kufanya mambo yote ambayo makuhani Walawi watawaagiza mfanye.^b Muwe waangalifu kufanya kama tu nilivyowaa-muru. **9** Kumbukeni jinsi Yehova Mungu wenu alivyomte-ndea Miriamu mlipokuwa njiani kutoka Misri.^c

10 “Ukimkopesha jirani yako kitu chochote,^d hupaswi kuingia nyumbani mwake ili kuchukua kitu anachotoa kuwa dhamana. **11** Unapaswa kusimama nje, na mtu huyo uliyemkopesha anapaswa kukuletea nje kitu anachotoa kuwa dhamana. **12** Na ikiwa mtu huyo ni maskini, hupaswi kulala na kitu alichokupa kuwa dhamana.^e **13** Unapaswa kufanya yote uwezayo kumrudishia kitu alichokupa kuwa dhamana baada tu ya jua kutua, naye atakuwa na vazi lake anapoenda kulala,^f na atakubariki; nawe utakuwa mwadilifu mbele za Yehova Mungu wako.

14 “Usimlaghai kibarua mwenye uhitaji na maskini, awe ni mmoja wa ndugu zako au ni mkaaji mgeni katika nchi yenu, ndani ya majiji* yenu.^g **15** Unapaswa kumpa mshahara wake siku hiyohiyo,^h kabla ya jua kutua, kwa sababu ana uhitaji na uhai

24:8 *Neno la Kiebrania linalotafsiriwa “ukoma” lina maana pana na lina-weza kutia ndani magonjwa mbalimbali ya ngozi yanayoambukiza. Linaweza pia kutia ndani maambukizi fulani yaliyopatikana kwenye nguo na nyumba. **24:14** *Tnn., “malango.”

SURA YA 24

a Kum 19:18, 19
Kum 21:20, 21

b Law 13:2, 15
Mk 1:44
Lu 17:14

c Hes 12:10, 15

d Kum 15:7, 8
Met 3:27

e Ayu 24:9, 10

f Kut 22:26, 27

g Law 25:39, 43
Met 14:31

h Law 19:13
Yer 22:13
Mt 20:8

Safu ya 2

a Met 22:22, 23
Yak 5:4

b 2Nya 25:3, 4

c Eze 18:20

d Kut 22:21, 22

e Kut 22:26, 27

f Kum 5:15

g Law 19:9
Law 23:22
Ru 2:16
Zb 41:1

h Kum 15:7, 10
Met 11:24
Met 19:17
Lu 6:38
2Ko 9:6
1Yo 3:17

i Law 19:10
Kum 26:13

wake unategemea* mshahara wake. Usipofanya hivyo, atamlilia Yehova, nawe utakuwa na hatia ya dhambi.^a

16 “Akina baba hawapaswi kuuawa kwa sababu ya dhambi za wana wao, na wana hawapaswi kuuawa kwa sababu ya dhambi za baba zao.^b Mtu anapaswa kuuawa kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe.^c

17 “Usipotoshe hukumu ya mkaaji mgeni au ya yatima,^d nawe hupaswi kuchukua vazi la mjane kuwa dhamana ya mkopo.*^e **18** Kumbukeni kwamba mlikuwa watumwa nchini Misri, na Yehova Mungu wenu akawakomboza kutoka huko.^f Ndiyo sababu ninawaamuru mfanye hivyo.

19 “Unapovuna mavuno yako shambani na kusahau tita shambani, usirudi kulichukua. Linapaswa kuachwa kwa ajili ya mkaaji mgeni, yatima, na mjane,^g ili Yehova Mungu wako akubariki katika kila jambo unalofanya.^h

20 “Unapoupiga mzeituni ili kuangusha zeituni, hupaswi kurudia kufanya hivyo kwenye matawi yake. Matunda yanayobaki utamwachia mkaaji mgeni, yatima, na mjane.ⁱ

21 “Unapokusanya zabibu katika shamba lako la mizabibu, hupaswi kurudi kukusanya zabibu zilizobaki. Unapaswa kumwachia mkaaji mgeni, yatima, na mjane. **22** Kumbukeni kwamba mlikuwa watumwa nchini Misri. Ndiyo sababu ninawaamuru mfanye hivyo.

24:15 *Au “nafsi yake inategemea.”

24:17 *Au “rehani.”

25 “Watu wakizozana, waweza kwenda kuwao-na waamuzi,^a nao wataamua kesi yao na kumtangaza mtu asiye na hatia kuwa mwadilifu na aliyi na hatia kuwa mwovu.^b **2** Ikiwa mtu mwovu anastahili kupigwa viboko,^c mwamuzi atamwagiza alale chini kifudufudi, na mtu huyo atapigwa viboko mbele yake. Idadi ya viboko inapaswa kulingana na uovu aliotenda. **3** Anaweza kumpiga kufikia viboko 40,^d lakini asizidishe. Akiendelea kumpiga viboko zaidi, ndugu yenu ataaibika machini penu.

4 “Hupaswi kumfunga kinywa ng’ombe dume anapopura nafaka.^e

5 “Ikiwa ndugu wanaishi pamoja na mmoja wao afe bila mwana, mke wa yule aliyekufa hapaswi kuolewa na mwanamume mwingine nje ya ukoo huo. Ndugu ya mume wake anapaswa kwenda kwake, amchukue awe mke wake, na kufunga naye ndoa ya ndugu mkwe.^f **6** Mtoto wa kwanza atakayemzaa ataendeleza jina la ndugu yake aliyekufa,^g ili jina lake lisifutiliwe mbali kutoka Israeli.^h

7 “Sasa ikiwa mwanamume huyo hataki kumwoa mjane wa ndugu yake, mjane huyo anapaswa kwenda kwa wazee kwenye lango la jiji na kuwaambia, ‘Ndugu ya mume wangu amekataa kuhifadhi jina la ndugu yake katika Israeli. Amekataa kufunga nami ndoa ya ndugu mkwe.’ **8** Ni lazima wazee wa jiji lake wamwite na kuzingumza naye. Ikiwa atasisitiza hivi: ‘Sitaki kumwoa,’ **9** basi mjane wa ndugu yake atamkaribia mbele ya

SURA YA 25

a Kum 16:18
Kum 17:8, 9
Kum 19:16, 17

b Kut 23:6
2Nya 19:6
Met 17:15
Met 31:9

c Met 10:13
Met 20:30
Met 26:3
Lu 12:48
Ebr 2:2

d 2Ko 11:24

e Met 12:10
IKo 9:9
ITI 5:18

f Mwa 38:7, 8
Ru 4:5
Mk 12:19

g Mwa 38:9
Ru 4:10, 17

h Hes 27:1, 4

Safu ya 2

a Ru 4:7

b Met 11:1
Met 20:10
Mik 6:11

c Law 19:36

d Kum 4:40

e Law 19:35

f Kut 17:8
Hes 24:20

wazee, atamvua mwanamume huyo kiatu,^a kisha amtemee mate usoni na kusema, ‘Hivyo ndivyo anavyopaswa kutendewa mwanamume ambaye hatajenga familia ya ndugu yake.’ **10** Kisha, jina la familia* yake katika Israeli litakuwa ‘Familia[#] ya mtu aliyevuliwa kiatu.’

11 “Wanaume wawili wikipigana na mke wa mmoja wao aingilie kati ili kumlinda mume wake asipigwe, naye aunyooshe mkono wake na kumkamata sehemu za siri mwanamume anayepigana na mume wake, **12** ni lazima mumkate mkono mwanamume huyo. Hampaswi* kumhurumia.

13 “Hupaswi kuwa na aina mbili za mawe ya mizani katika mfuko wako,^b jiwe kubwa na dogo. **14** Hupaswi kuwa na aina mbili za vyo-mbo vya kupimia*^c nyumbani mwako, kikubwa na kidogo. **15** Unapaswa kuwa na mawe ya kupimia yaliyo sahihi na ya haki na kipimo kilicho sahihi na cha haki, ili uendelee kuishi kwa muda mrefu katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa.^d **16** Kwa maana kila mtu asiyetenda haki ambaye anafanya mambo hayo ni chukizo kwa Yehova Mungu wenu.^e

17 “Kumbukeni yale ambayo Waamaleki waliwatendea mlipokuwa njiani kutoka Misri,^f **18** jinsi walivyokutana nanyi njiani na kuwashambulia wale wote waliokuwa wakijikokota nyuma mlipokuwa

25:10 *Au “jina la nyumba.” Tnn., “jina lake.” #Tnn., “Nyumba.” 25:12 *Tnn., “Jicho lenu halipaswi.” 25:14 *Tnn., “efa na efa.” Angalia Nyongeza B14.

mmechoka na kuishiwa nguvu. Hawakumwogopa Mungu. **19** Yehova Mungu wenu atakapokuwa amewapumzisha kutokana na maadui wenu wote wanaowazunguka katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa kuwa urithi ili mwimiliki,^a mnapaswa kuwaangamiza kabisa Waamaleki ili wasikumbukwe tena chini ya mbingu.^b Msisahau jambo hilo.

26 “Mwishowe mtakapoingia katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa kuwa urithi wenu, nanyi mmeimiliki na mnaishi ndani yake, **2** mtachukua baadhi ya mavuno ya kwanza ya mazao* yote ya ardhi, mtakayokusanya katika nchi yenu ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, na kuyatia katika kipapu na kwenda mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua jina lake likae hapo.^c **3** Mtaenda kwa kuhani atakayekuwa akihudumu wakati huo na kumwambia, ‘Leo nimekuja kumjulisha Yehova Mungu wako kwamba nimeingia katika nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zetu kwamba atatupa sisi.’^d

4 “Kisha kuhani atachukua kikapu hicho kutoka mkononi mwako na kukiweka mbele ya madhabahu ya Yehova Mungu wako. **5** Halafu utatanga hivi mbele za Yehova Mungu wako: ‘Baba yangu alikuwa Mwaramu aliyekuwa akitungatanga,^{*e} akashuka kwenenda Misri^f na kukaa huko akiwa mgeni, akiwa na watu wachache wa familia yake.’^g

26:2 *Tnn., “matunda.” 26:5 *Au labda, “akiangamia.”

SURA YA 25

a Yos 22:4

b Kut 17:14
1Sa 14:47, 48
1Sa 15:1-3
1Nya 4:42, 43

SURA YA 26

c Kut 23:19
Law 23:10
Hes 18:8, 12
2Nya 6:6
2Nya 31:5
Met 3:9d Mwa 17:1, 8
Mwa 26:3e Mwa 28:5
Ho 12:12f Mwa 46:3
Mdo 7:15

g Mwa 46:27

Safu ya 2

a Kut 1:7
Kum 10:22
Zb 105:24

b Kut 1:11

c Kut 3:9
Kut 4:31
Mdo 7:34

d Kut 6:6

e Kut 7:3
Kum 4:33, 34f Kut 3:8
Kum 8:7, 8
Eze 20:6

g Kum 26:2

h Kum 12:7
Kum 16:14i Kum 12:5, 6
Kum 14:22j Kum 14:28, 29
Met 14:21
1Yo 3:17

k Yak 1:27

Lakini huko akawa taifa kubwa, lenye nguvu na lenye watu wengi.^a **6** Na Wamisri wakatutesa na kutukandamiza na kututumikisha kikati-li.^b **7** Basi tukaanza kumlilia Yehova, Mungu wa mababu zetu, naye Yehova akasikia sauti yetu na kutazama mateo yetu na taabu yetu na kukandamizwa kwetu.^c **8** Mwishowe Yehova akatutoa Misri kwa mkono wenye nguvu na mkono ulionyoochwahwa^d na kwa matendo yanayotisha na kwa ishara na miujiza.^e **9** Kisha akatuleta mahali hapa na kutupatia nchi hii, nchi inayotiririka maziwa na asali.^f **10** Sasa nimeleta mavuno ya kwanza ya mazao ya ardhi ambayo Yehova amenipa.^g

“Ni lazima ukiweke kikapu hicho mbele za Yehova Mungu wako na kuinama mbele za Yehova Mungu wako. **11** Kisha utashangilia kwa sababu ya vitu vyote vyema ambavyo Yehova Mungu wako amekupa wewe na nyumba yako, wewe na Mlwi na mkaaji mgeni aliyemiongoni mweni.^h

12 “Baada ya kutoa sehemu yote ya kumiⁱ ya mazao yako katika mwaka wa tatu, mwaka wa sehemu ya kumi, utampa sehemu hiyo Mlwi, mkaaji mgeni, yatima, na mjane, nao watakula na kushiba katika majiji*^j yenu. **13** Kisha utasema hivi mbele za Yehova Mungu wako: ‘Nimeondoa sehemu takatifu kutoka katika nyumba yangu na kumpa Mlwi, mkaaji mgeni, yatima, na mjane,^k kama ulivyoni muru. Sijavunja wala kupuza amri zako. **14** Sikuila nikiombole-

26:12 *Tnn., “malango.”

za wala kutoa kisehemu chochote nikiwa mchafu au kutoa kisehemu chochote kwa ajili ya wafu. Nimetii sauti ya Yehova Mungu wangu na kufanya mambo yote uliyoniamuru. **15** Sasa tazama chini kutoka katika makao yako matakatifu, mbinguni, na kuwabariki watu wako Waisraeli na nchi ambayo umetupatia,^a kama ulivyowaapia mababu zetu,^b nchi inayotiririka maziwa na asali.^c

16 “Siku ya leo Yehova Mungu wako anakuumuru utekeleze masharti haya na sheria hizi.* Ni lazima uzishike na kuzitekeleza kwa moyo wako wote^d na nafsi^e yako yote. **17** Leo Yehova amewatanzia kwamba atakuwa Mungu wenu mnapotembea katika njia zake na kushika masharti yake,^e amri zake,^f na sheria zake,^g na mnaposikiliza sauti yake. **18** Na leo mmemtangazia Yehova kwamba mtakuwa watu wake, mali yake ya pekee,^h kama alivyowaahidi, na kwamba mtashika amri zake zote **19** na kwamba atawakweza juu ya mataifa mengine yote ambayo ameyatokeza,ⁱ akiwapa sifa na umaarufu na utukufu mnapothibitisha kwamba ninyi ni taifa takatifu kwa Yehova Mungu wenu,^j kama alivyoahidi.”

27 Kisha Musa pamoja na wazee wa Israeli wakawaamuru watu hivi: “Shikeniki kila amri ninayowapa leo. **2** Na siku mtakayovuka Yordani kuingia katika nchi

26:16 *Tnn., “maamuzi haya ya hukumu.” #Angalia Kamusi, uku. 2012. 26:17 *Tnn., “maamuzi yake ya hukumu.” 26:18 *Au “mali yake anayothamani sana.”

SURA YA 26

a Kut 23:25

b Mwa 15:18
Mwa 26:3

c Kum 8:7,8

d Kum 6:6
Kum 11:1
Zb 119:34
1Yo 5:3

e Law 26:46

f Mhu 12:13

g Law 19:37

h Kum 14:2
Kum 29:10-13

i Kum 4:8

j Kum 7:6
Kum 28:1,9

Safu ya 2

SURA YA 27

a Yos 8:30-32

b Hes 13:26,27

c Kum 11:29

d Kut 20:25

e Law 3:1

f Law 7:15

g Kum 12:7

h Kut 24:12

i Kut 19:5
Kum 26:18j 1Fa 2:3
Mt 19:17
1Yo 5:3

k Kum 11:29

ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, mtapanga mawe makubwa na kuyapaka cho-kaa.*^a **3** Kisha mwandike juu yake maneno yote ya Sheria hii mtakapokuwa mmevuka, ili muweze kuingia katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa, nchi inayotiririka maziwa na asali, kama Yehova Mungu wa mababu zenu alivyowaahidi.^b **4** Mtakapokuwa mmevuka Yordani, mnapaswa kupanga mawe hayo kwenye Mlima Ebali^c na kuyapaka chokaa,* kama ninavyowaamuru leo. **5** Pia mtamjengea Yehova Mungu wenu madhabahu huko, madhabahu ya mawe. Msitumie vifaa vya chuma kuijenga.^d **6** Mnapaswa kuijenga madhabahu ya Yehova Mungu wenu kwa mawe ambayo hayajachongwa na kumtolea Yehova Mungu wenu dhabihu za kuteketezwa juu yake. **7** Mtatoa dhabihu za ushirika^e na kuzila mahali hapo,^f nanyi mtashangilia mbebe za Yehova Mungu wenu.^g **8** Andikeni waziwazi maneno yote ya Sheria hii juu ya mawe hayo.”^h

9 Kisha Musa na makuhani Walawi wakawaambia hivi Waisraeli wote: “Nyamazeni, msikilize, enyi Waisraeli. Siku ya leo mmekuwa watu wa Yehova Mungu wenu.ⁱ **10** Ni lazima msikilize sauti ya Yehova Mungu wenu na kutekeleza amri zake^j na masharti yake, nina-yyaamuru leo.”

11 Siku hiyo Musa akawaamuru watu hivi: **12** “Makabila yafuatayo yatasimama kwenye Mlima Gerizimu^k ili kuwabariki watu mtakapokuwa

27:2, 4 *Au “kuyapiga lipu.”

mmevuka Yordani: Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, Yosefu, na Benjamini. **13** Na makabila yafuatayo yatasimama kwenye Mlima Ebali^a ili kutangaza laana: Rubeni, Gadi, Asheri, Zabuloni, Dani, na Naftali. **14** Na Walawi watamwambia hivi kila Mwisraeli kwa sauti kubwa:^b

15 “Amelaaniwa mtu anayetengeneza sanamu ya kuchongwa^c au sanamu ya chuma,^{*d} kitu kinachomchukiza Yehova,^e kilichotengenezwa na mikono ya fundi,[#] na ambaye amekificha.’ (Na watu wote watasema, ‘Amina!’^Δ)

16 “Amelaaniwa mtu anayemharau baba yake au mama yake.’^f (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

17 “Amelaaniwa mtu anayesogeza alama ya mpaka wa jirani yake.’^g (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

18 “Amelaaniwa mtu anayemfanya kipofu apotee njia.’^h (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

19 “Amelaaniwa mtu anayepotosha hakiⁱ ya mkaaji mgeni, yatima, au mjane.’^j (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

20 “Amelaaniwa mtu anayefanya ngono na mke wa baba yake, kwa sababu amewaibisha baba yake.’^{**k} (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

21 “Amelaaniwa mtu anayefanya ngono na mnyama yeyote.’^l (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

27:15 *Au “sanamu ya kuyeyushwa.”
^aAu “fundu wa mbao na chuma.” ^ΔAu
 “Na iwe hivyo!” 27:20 *Tnn., “amemfuna
 nua nguo baba yake.”

SURA YA 27

a Yos 8:33

b Kum 33:10

c Kut 20:4
Kum 4:15, 16
Isa 44:9d Kut 34:17
Law 19:4e Kum 7:25
Kum 29:17f Kut 20:12
Kum 21:18-21
Met 20:20
Met 30:17
Mt 15:4g Kum 19:14
Met 23:10

h Law 19:14

i Kum 16:20
Met 17:23
Mik 3:11j Kut 22:21, 22
Kum 10:17, 18
Mal 3:5
Yak 1:27k Law 18:8
1Ko 5:1l Kut 22:19
Law 18:23
Law 20:15

Safu ya 2

a Law 18:9
Law 20:17b Law 18:17
Law 20:14c Kut 20:13
Kut 21:12
Hes 35:31

d Mt 27:3, 4

e Kum 28:15
Gal 3:10

SURA YA 28

f Kum 26:18, 19

g Law 26:3, 4
Met 10:22
Isa 1:19

h Kum 11:14

i Law 26:9
Zb 127:3
Zb 128:3

j Kum 7:13

k Kum 26:2

l Kut 23:25

22 “Amelaaniwa mtu anayefanya ngono na dada yake, binti ya baba yake au binti ya mama yake.’^a (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

23 “Amelaaniwa mtu anayefanya ngono na mama mkwe wake.’^b (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

24 “Amelaaniwa mtu anayemviza na kumuua jirani yake.’^c (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

25 “Amelaaniwa mtu anayekubali rushwa ili amuue mtu asiye na hatia.’^d (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

26 “Amelaaniwa mtu ambaye hataunga mkono maneno haya ya Sheria kwa kuyatekeleza.’^e (Na watu wote watasema, ‘Amina!’)

28 “Nanyi kwa hakika mkiisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu kwa kuwa waangalifu kutenda amri zake zote ninazowaamuru leo, kwa hakika Yehova Mungu wenu atawakweza juu ya mataifa mengine yote ya dunia.’^f

2 Baraka hizi zote zitawajia na kuwatangulia,^g kwa sababu mnaendelea kuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu:

3 “Mtabarikiwa jijini na mtabarikiwa shambani.^h

4 “Watoto wenu^{*} watabarikiwa na pia mazao ya ardhi yenu na watoto wa mifugo yenu, ng’ombe wenu wachanga na wanakondoo wenu.^l

5 “Kikapu chenu^k na bakuli lenu la kukandia litabarikiwa.^l

6 “Mtabarikiwa mnapoingia ndani, na mtabarikiwa mnapotoka nje.

7 “Yehova atafanya maaudui wanaowashambulia wa-

28:4 *Tnn., “Wazao wa tumbo lenu.”

shindwe mbele yenu.^a Watawashambulia kutoka upande mmoja, lakini watawakimbia wakielekea pande saba tofauti.^b **8** Yehova atawaagizia baraka katika maghala yenu^c na katika kila kazi mnyafanya, na kwa hakika atawabariiki katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa. **9** Yehova atawafanya kuwa taifa lake takatifu,^d kama alivyowaapia,^e kwa sababu mnaendelea kushika amri za Yehova Mungu wenu na kutembea katika njia zake. **10** Mataifa yote duniani yatalazimika kuona kwamba mmeitwa kwa jina la Yehova,^f nayo yatawaogopa ninini.^g

11 “Yehova atawafanya muwe na watoto wengi sana na mifugo mingi sana na mazao mengi sana^h katika nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zenu kwamba atawapa ninini.ⁱ **12** Yehova atawafungulia ghala lake zuri, mbingu, ili mvua inyeshe juu ya nchi yenu katika majira yake^j na kubariki kila jambo mnalofanya. Mtayakopesha mataifa mengi, lakini ninii wenyewe hamtahitaji kukopa.^k **13** Yehova atawafanya kuwa kichwa juu^l wala si chini, mkiendelea kutii amri za Yehova Mungu wenu ninazowaamuru leo mzihsike na kuzitenda. **14** Msi-kengeuke kutoka katika maneno yote ninayowaamuru ninii leo, na kwenda kulia au kushoto,^m kwa kufuata miungu mingine ili kuiabudu.ⁿ

15 “Lakini msipoisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu kwa kuwa waangalifu kute-nda amri zake zote na sheria

SURA YA 28

a Kum 32:30
Yos 10:11

b Kum 7:23
2Nya 14:13

c Law 26:10
Met 3:9,10
Mal 3:10

d Kum 7:6

e Kut 19:6

f Isa 43:10
Da 9:19
Mdo 15:17

g Hes 22:3
Kum 11:25
Yos 5:1

h Kum 30:9
Zb 65:9

i Mwa 15:18

j Law 26:4
Kum 11:14

k Kum 15:6

l 1Fa 4:21

m Kum 5:32
Yos 1:7
Isa 30:21

n Law 19:4

Safu ya 2

a Law 26:16,17
Da 9:11

b 1Fa 17:1

c Kum 26:2

d Law 26:26

e Omb 2:11,19
Omb 4:10

f Law 26:20,22

g Yos 23:16

h Law 26:25
Yer 24:10

i Law 26:16

j Law 26:33

k Amo 4:9

l Law 26:19
Kum 11:17
1Fa 17:1

m Law 26:14,17
1Sa 4:10

n Yer 29:18
Lu 21:24

zake ninazowaamuru leo, laa-na hizi zote zitawajia na kuwatangulia.^a

16 “Mtalaaniwa jijini na mtalaaniwa shambani.^b

17 “Kikapu chenu^c na bakuli lenu la kukandia^d vitalaaniwa.

18 “Watoto wenu^e na mazao ya ardhi yenu na ng’ombe wenu wachanga na wanakondoo wenu watalaaniwa.^f

19 “Mtalaaniwa mnapoingia ndani na mtalaaniwa mnapotoka nje.

20 “Yehova atawaletea laana, vurugu na adhabu katika kila kazi mnyafanya mpaka mtakapoangamizwa na kutoweka upesi, kwa sababu ya mazoea yenu maovu na kuniacha mimi.^g **21** Yehova atafanya magonjwa yawaandame mpaka atakapokuwa amewaangamiza kutoka katika nchi mnyoenda kumiliki.^h **22** Yehova atawapiga kwa kifua kikuu, homa kali,ⁱ mwasho, joto la homa, upanga,^j upepo unaocho-ma, na kuvu;^k navyo vitawaandama mpaka mtakapoangamia. **23** Anga lililo juu ya vichwa vyenu litakuwa shaba, na dunia iliyo chini yenu itakuwa chuma.^l **24** Yehova atafanya mvua ya nchi yenu iwe ungaunga na mavumbi ambayo yatawanyeshea kutoka mbinguni mpaka mtakapoangamia kabisa. **25** Yehova atafanya mshindwe mbele ya maadui wenu.^m Mtawashambulia kutoka upande mmoja, lakini mtawakimbia mkielekea pande saba tofauti; nanyi mtakuwa kitu cha kutisha kwa falme zote za dunia.ⁿ **26** Na maiti

28:18 * Tnn., “Wazao wa tumbo lenu.”

zenu zitakuwa chakula kwa kila ndege wa angani na mnyama wa ardhini, na hakuna mtu atakayewafukuza.^a

27 “Yehova atawapiga kwa majipu ya Misri, bawasiri, ukurutu, na upele wa ngozi, nanyi hamtaweza kupona magonjwa hayo. **28** Yehova atawaletea kichaa na upofu^b na kuwafanya mchanganyikiwe.*

29 Mtapapasa-papasa wakati wa adhuhuri, kama kipofu anavyopapasa-papasa gizani,^c nanyi hamtafanikiwa katika jambo lolote mnalofanya; na watu watawalaghai na kuwanyang'anya vitu vyenu daima, na hakuna atakayewaokoa.^d

30 Utamchumbia mwanamke, lakini mwanamume mwingine atambaka. Utajenga nyumba, lakini hutaishi ndani yake.^e Utapanda shamba la mizabibu, lakini hutaanza kula matunda yake.^f **31** Ng'ombe dume wako atachinjwa mbele ya macho yako, lakini hutakula nyama yake. Punda wako ataubwa mbele ya macho yako, lakini hatarudishwa. Maadui wako watapewa kondoo wako, lakini hakuna atakayekusaidia. **32** Watu wengine watapewa wana wako na mabinti wako^g huku ukitazama, na sikuzote utatamani kuwaona, lakini mikono yako haitakuwa na nguvu za kufanya chochote. **33** Mavuno ya ardhi yako na mazao yako yote yataliwa na watu usiowajua,^h na sikuzote watu watawalaghai na kuwakandamiza. **34** Mtashikwa na kichaa kwa sababu ya mambo mtakayoona kwa macho yenu.

35 “Yehova atayapiga magoti yenu na miguu yenu kwa

28:28 *Au “mvurugike moyoni.”

SURA YA 28

a Yer 7:33

b Kut 4:11

c Isa 59:10

d Amu 3:14
Amu 6:1-5
Ne 9:27

e Isa 5:9
Omb 5:2

f Amo 5:11
Mik 6:15

g 2Nya 29:9

h Ne 9:37
Isa 1:7

Safu ya 2

a 2Fa 17:6
2Fa 25:7
2Nya 33:11
2Nya 36:5, 6

b Yer 16:13

c 1Fa 9:8
2Nya 7:20
Yer 24:9
Yer 25:9

d Isa 5:10
Hag 1:6

e Sef 1:13

f 2Fa 24:14
Yer 52:15, 30

g Met 22:7

h Ezr 9:7

i Kum 28:15
Kum 29:27

j 2Fa 17:20
Yer 24:10

majipu yenye maumivu makali na yasiyopona, kuanzia nyayo za miguu yenu mpaka utosini.

36 Yehova atawapeleka ninyi na mfalme mliyemchagua awe juu yenu, kwenye taifa ambalo ninyi hamlijui wala mababu zenu hawakulijua,^a na huko mtaabudu miungu mingine, miungu ya miti na ya mawe.^b

37 Nanyi mtakuwa kitu cha kutisha na cha kudharauliwa,* na kitu cha kudhiihakiwa miongoni mwa mataifa yote ambako Yehova atawapeleka.^c

38 “Mtapanda mbegu nyingi shambani, lakini mtavuna mazao machache,^d kwa sababu nzige watayala. **39** Mtapanda na kupalilia mashamba ya mizabibu, lakini hamtakunywa divai kamwe wala kukusanya zabibu zozote,^e kwa sababu kiwavi atazila. **40** Mtakuwa na mizeituni katika eneo lenu lote, lakini hamtajipaka mafuta yoyote, kwa sababu zeituni zenu zitaanguka. **41** Mtazaa wana na mabinti, lakini hawataendelea kuwa wenu, kwa sababu watapelekwa utekwani.^f

42 Makundi ya wadudu* yatavamia miti yenu yote na mazao ya ardhi yenu. **43** Mkaaji mgeni aliye miongoni mwenu ataendelea kupanda juu yenu zaidi na zaidi, huku ninyi mkiendelea kushuka chini zaidi na zaidi. **44** Atawakopesha, lakini ninyi hamtamkopesha.^g Atakuwa kichwa, lakini ninyi mtakuwa mkia.^h

45 “Laana hizi zoteⁱ hakika zitawajia na kuwafuatia na kuwatangulia mpaka mtakapokuwa mmeangamizwa,^j kwa sababu hamkuisikiliza sauti ya

28:37 *Tnn., “methali.” 28:42 *Au “Wadudu wanaoruka.”

Yehova Mungu wenu kwa ku-shika amri zake na sheria zake alizowaamuru.^a **46** Nazo zi-taendelea kuwaandama ninyi na wazao wenu kama ishara na dalili ya kudumu,^b **47** kwa sababu hamkumtumikia Yehova Mungu wenu kwa furaha na shangwe moyoni mlipokuwa na wingi wa kila kitu.^c **48** Yehova atawatuma maadui wenu wawashambulie, nanyi mtawatumikia^d mkiwa na njaa^e na kiu na uchi na mkiwa maskini kabisa.* Ataweka nira ya chuma kwenye shingo zenu mpaka atakapokuwa amewaangamiza.

49 "Yehova ataleta dhidi yenu taifa la mbali,^f kutoka mwisho wa dunia; litawarukia kama tai,^g taifa ambalo hamtaelewa lugha yake,^h **50** taifa lenye uso mkali ambalo haliwajali wazee wala kuwahurumia vijana.ⁱ **51** Watu hao watawala watoto wa mifugo yenu na mazao ya ardhi yenu mpaka mtakapokuwa mmeangamizwa. Hawatawaachia nafaka yoyote, divai mpya wala mafuta, ng'ombe mchanga wala mwanakondoo mpaka watakapokuwa wamewaangamiza.^j **52** Watawazingira na kuwafungia ndani ya majiji* yenu yote, katika nchi yenu yote, mpaka kuta zenu ndefu na zenye ngome mna-zozitegemea zitakapoanguka. Naam, kwa hakika watawazingira katika majiji yenu yote, katika nchi yenu yote ambayo Yehova Mungu wenu amewapa ninyi.^k **53** Ndipo mtakapolazimika kuwala watoto wenu*

28:48 *Au "bila kitu chochote." **28:52** *Tnn., "malango." **28:53** *Tnn., "wazao wa tumbo lenu."

SURA YA 28

a Kum 11:26-28

b 1Ko 10:11

c Kum 12:7
Ne 9:35d 2Nya 12:8, 9
Yer 5:19

e Yer 44:27

f Yer 6:22
Hab 1:6g Yer 4:13
Ho 8:1

h Yer 5:15

i 2Nya 36:17
Isa 47:6
Lu 19:44j Law 26:26
Yer 15:13k 2Fa 17:5
2Fa 25:1
Lu 19:43

Safu ya 2

a 2Fa 6:28
Omb 4:10
Eze 5:10

b Yer 52:6

c Omb 4:5

d Kut 24:7
Kum 31:26e Kum 10:17
Zb 99:3f Kut 3:15
Kut 6:3
Kut 20:2
Zb 83:18
Zb 113:3
Isa 42:8g Law 26:21
Da 9:12

wenyewe, nyama ya wana wenu na mabinti wenu^a ambao Yehova Mungu wenu amewapa, kwa sababu ya kuzingirwa kabisa na kwa sababu ya mateso yata kayosababishwa na adui yenu.

54 "Hata mwanamume mpole sana na aliyedekezwa miongoni mwenu hatamhurumia ndugu yake au mke wake mpendwa au wanawe wanaobaki, **55** naye hatawagawia hata kidogo nyama ya wanawe ambayo atakula, kwa sababu hana kitu kingine chochote cha kula kwa sababu ya kuzingirwa kabisa na kwa sababu ya mateso yata kayosababishwa na adui yenu katika majiji yenu.^b **56** Na mwanamke mpole sana na aliyedekezwa miongoni mwenu ambaye hata hawezi kuthubutu kukanyaga chini kwa wayo wa mguu wake kwa sababu ya kudekeza sana^c hatamhurumia mume wake mpendwa wala mwanawe wala binti yake, **57** wala hata kondo la nyuma linalotoka katikati ya miguu yake wala wana anaozaa, kwa sababu atawala kwa siri kwa sababu ya kuzingirwa kabisa na kwa sababu ya mateso yata kayosababishwa na adui yenu katika majiji yenu.

58 "Ikiwa hamtashika kwa uangalifu maneno yote ya Sheria hii ambayo yameandikwa katika kitabu hiki^d na msipoliogopa jina hili tuku-fu na lenye kuogopesha,^e la Yehova^f Mungu wenu, **59** Yehova atawatesa ninyi na wazao wenu kwa mapigo makali sana, mapigo makubwa yanayodumu,^g na magonjwa hatari yanayodumu. **60** Atawaletea

tena magonjwa yote ya Misri mliyokuwa mkiogopa, nayo kwa hakika yatawaandama ninyi. **61** Isitoshe, Yehova atawaletea pia kila ugonjwa au pigo ambalo halijaandikwa katika kitabu hiki cha Sheria mpaka mtakapoangamia. **62** Ingawa mmekuwa wengi sana kama nyota za mbinguni,^a ni wachache sana miongoni mweni watakaobaki,^b kwa sababu hamkuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu.

63 “Na kama Yehova alivyopendezwa wakati mmoja kuwafanikisha na kuwafanya mwongezeke, ndivyo Yehova atakavyopendezwa kuwaharibu na kuwaangamiza; nanyi mtang’olewa kutoka katika nchi mnayokaribia kumiliki.

64 “Yehova atawatawanya miongoni mwa mataifa yote, kutoka mwisho mmoja wa dunia mpaka mwisho mwingine wa dunia,^c na huko mtalazimika kuabudu miungu ya miti na mawe, ambayo wala ninyi wala mababu zenu hamwijui.^d **65** Hamtakuwa na amani miongoni mwa mataifa hayo^e wala mahali pa kupumzisha wayo wa mguu wenu. Badala yake, mkiwa huko Yehova atawapa moyo wenye mahangai-ko^f na macho yanayodhoofika na hisia za kukata tamaa.^{*g} **66** Uhai wenu utakabili hatari kubwa, nanyi mtaogopa usiku na mchana; nanyi hamtakuwa na uhakika wa kuokoka. **67** Asubuhi mtasema, ‘Laiti ingekuwa jioni!’ na jioni mtasema, ‘Laiti ingekuwa asubuhi!’ kwa sababu ya woga mtakaohisi mioyoni mweni na

SURA YA 28

a Kum 10:22

b Kum 4:27

c Law 26:33
Ne 1:8
Lu 21:24

d Kum 4:27, 28

e Amo 9:4

f Eze 12:19

g Law 26:16, 36

Safu ya 2

SURA YA 29

a Kut 24:8

b Kut 19:4
Yos 24:5c Kum 4:34
Ne 9:10

d Ro 11:8

e Kum 1:3
Kum 8:2f Kum 8:4
Ne 9:21
Mt 6:31

g Hes 21:26

h Hes 21:33

i Zb 135:10, 11

kwa sababu ya mambo ambayo macho yenu yataona. **68** Na hakika Yehova atawarudisha Misri kwa meli, kupitia ile njia niliyowaambia hivi kuhusu: ‘Hamtaiona tena kamwe,’ na huko mtalazimika kujiuza kwa maadui wenu ili kuwa watumwa wa kiume na wa kike, lakini hakutakuwa na mtu wa kuwanunua.”

29 Haya ndiyo maneno ya agano ambalo Yehova alimwamuru Musa afanye pamoja na Waisraeli katika nchi ya Moabu, mbali na agano alilofanya nao kule Horebu.^a

2 Kisha Musa akawaita Waisraeli wote na kuwaambia, “Mmeona mambo yote ambayo Yehova alifanya mbele ya macho yenu katika nchi ya Misri, mambo ambayo alimtendea Farao na watumishi wake wote na nchi yake yote,^b **3** hukumu kubwa ambazo* macho yenu yaliona, zile ishara kubwa na miujiza.^c **4** Lakini mpaka leo hii Yehova hajawapa moyo wa kuelewa na macho ya kuona na masikio ya kusikia.^d **5** ‘Nilipokuwa nikiwaongoza kwa miaka 40 nyikani,^e nguo mlizovaa hazikuchakaa na viatu mliyovaa havikuchakaa miguuni mwenu.^f **6** Hamkula mkate wala kunywa divai wala kinywaji chochote chenye kileo, ili mjue kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu.’ **7** Mwishowe mkafika mahali hapa, na Sihoni mfalme wa Heshboni^g na Ogu mfalme wa Bashani^h wakaja kupigana nasi, lakini tukawashinda.ⁱ **8** Baada ya hayo tukachukua nchi yao na kuwapa Warubeni, Wagadi,

28:65 * Au “nafsi iliyokata tamaa.”

29:3 * Au “majaribu makubwa ambayo.”

na nusu ya kabila la Manase iwe urithi wao.^a **9** Kwa hiyo, shikeni maneno ya agano hili na kuyatii, ili kila jambo mna- lofanya lifanikiwe.^b

10 “Leo ninyi nyote mmesi- mama mbele za Yehova Mungu wenu; viongozi wa makabila yenu, wazee wenu, maofisa wenu, kila mwanamume wa Israeli, **11** watoto wenu, wake zenu,^c na mkaaji mgeni^d anayeishi kambiini mweni, kuanzia mtu anayewakusanyia kuni mpaka anayewatekea maji. **12** Mko hapa ili mwingie katika agano la Yehova Mungu wenu na kiapo chake, agano ambalo Yehova Mungu wenu anafanya pamoja nanyi leo^e **13** ili leo awafanye ninyi kuwa watu wake^f na ili awe Mungu wenu,^g kama alivyowaahidi ninyi na kama alivyowaapita mababu zenu, Abrahamu,^h Isaka,ⁱ na Yakobo.^j

14 “Sasa sifanyi agano hili na kiapo hiki pamoja nanyi tu, **15** bali nafanya pamoja na ninyi mnaosimama hapa pamoja nasi leo mbele za Yehova Mungu wetu na pamoja na wale ambao leo hawapo hapa pamoja nasi. **16** (Kwa maana ninyi mnajua vizuri jinsi tulivyoishi nchini Misri na jinsi tulivyopita katikati ya mataifa mbalimbali tulipokuwa safarini.^k **17** Nanyi mlikuwa mkiona vitu vyao vinavyochukiza na sanamu zao zenye kuchukiza*^l za miti na mawe, fedha na dhahabu, walizokuwa nazo.) **18** Jihadharini ku- siwe na mwanamume au mwanamke, familia au kabila lolo-

29:17 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

SURA YA 29

a Hes 32:33
Kum 3:12, 13

b Kum 4:6
Kum 8:18
Yos 1:7, 8
1Fa 2:3
Zb 103:17, 18
Lu 11:28

c Ne 8:2

d Kut 12:38

e Kum 1:3
Kum 29:1

f Kut 19:5
Kum 7:6
Kum 28:9

g Kut 6:7
Kut 29:45

h Mwa 17:1, 7
Mwa 22:16, 17

i Mwa 26:3

j Mwa 28:13

k Kum 2:4

l Hes 25:1, 2

Safu ya 2

a Kum 11:16
Ebr 3:12

b Ebr 12:15

c Yos 24:19

d Kum 27:26
Kum 28:15

e Mwa 19:24
Yud 7

f Mwa 10:19
Mwa 14:2

te kati yenu leo ambalo moyo wake utageuka na kumwacha Yehova Mungu wetu ili kwenda kuabudu miungu ya mataifa hayo,^a ili miongoni mweni ku- siwe na mzizi unaozaa tunda lenye sumu na pakanga.^b

19 “Lakini mtu akisikia maneno ya kiapo hiki na kuji- gamba moyoni mwake akise- ma, ‘Nitakuwa na amani, inga- wa ninasisitiza kwamba nitae- ndelea kutembea katika njia za moyo wangu mwenyewe,’ na hivyo kuharibu kila kitu* kilicho kwenye njia yake, **20** Yehova hatakuwa tayari kumsamehe.^c Badala yake, ha- sira kali ya Yehova itawaka dhidi ya mtu huyo, na laana yote iliyoandikwa katika ki- tabu hiki hakika itampata,^d na Yehova kwa kweli atafuti- lia mbali jina la mtu huyo ku- toka duniani.* **21** Kisha Ye- hova atamenga kutoka katika makabila yote ya Waisraeli ili apate msiba kulingana na la- ana yote ya agano iliyoandikwa katika kitabu hiki cha Sheria.

22 “Kizazi cha wakati ujao cha wana wenu na pia wage- ni kutoka nchi za mbali wata- kapoona mapigo ya nchi, ma- gonjwa ambayo Yehova ame- leta juu yake— **23** kiberiti na chumvi na kuteketea, hivi kwamba nchi yote haitapa- ndwa wala kuchiputa mimea, wala hakuna mmea wowote utakaoota ndani yake, kama ilivyokuwa wakati wa ma- ngamizi ya Sodoma na Gomo- ra,^e Adma na Seboiimu,^f majiji ambayo Yehova aliyangamiza katika hasira yake na katika

29:19 *Tnn., “kitu kilichonyeshwa maji vizuri pamoja na kitu kilichokauka.”

29:20 *Tnn., “chini ya mbingu.”

ghadhabu yake— **24** wao pamoja na mataifa yote watauliza, ‘Kwa nini Yehova aliitendea hivi nchi hii?’^a Ni nini kilichomfanya awake hasira kali hivi?’ **25** Kisha wataseka, ‘Ni kwa sababu walilicha agano la Yehova,^b Mungu wa mababu zao, ambalo alifanya pamoja nao alipowatoa nchini Misri.’^c **26** Lakini walienda na kuabudu miungu mingine na kuinamia, miungu ambayo hawakuwa wameijua na ambayo hakuwaruhusu waiabudu.* **27** Ndipo hasira kali ya Yehova ikawaka dhidi ya nchi hiyo, naye akailitea nchi hiyo laana yote iliyoandikwa katika kitabu hiki.^e **28** Kwa hiyo, Yehova akawang’oa kutoka katika ardhi yao kwa hasira yake^f na ghadhabu kali na hamaki na kuwapeleka katika nchi nyingine, mahali walipo mpaka leo.’^g

29 “Mambo yaliyofichwa ni ya Yehova Mungu wetu,^h lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu na wazao wetu milele, ili tutekeleze maneno yote ya Sheria hii.’ⁱ

30 “Maneno haya yote yatakapotimia kwenu, baraka na laana ambayo nimeweka mbele yenu,^j nanyi myakumbuke*^k katika mataifa yote ambako Yehova Mungu wenu atawatawanya,^l **2** nanyi mrudi kwa Yehova Mungu wenu^m na kuisikiliza sauti yake kulingana na yote ninayowaamuru leo, ninyi na wana wenu, kwa moyo wenu wote na kwa nafsi* yenu yote,ⁿ **3** ndipo Yehova Mungu wenu atakapowarudi-

29:26 *Au “hakuwapa.” 30:1 *Tnn., “myatie tena moyoni mwenu.” 30:2, 6, 10 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 29

- a 1Fa 9:8, 9
2Nya 7:21, 22
Yer 22:8, 9
- b 1Fa 19:10
- c Yer 31:32
- d Amu 2:12
- e Law 26:16
Kum 27:26
- f Kum 28:45, 63
1Fa 14:15
2Fa 17:18
Lu 21:24
- g Ezz 9:7
Da 9:7
- h Ro 11:33
- i Zb 78:5
Mhu 12:13

SURA YA 30

- j Kum 11:26-28
Kum 28:2, 15
- k 1Fa 8:47
Ne 1:9
Eze 18:28
Yoe 2:13
- l 2Fa 17:6
2Nya 36:20
- m Isa 55:7
1Yo 1:9
- n Kum 4:29

Safu ya 2

- a Yer 29:14
- b Omb 3:22
- c Ezz 1:2, 3
Zb 147:2
Yer 32:37
Eze 34:13
- d Kum 28:64
Sef 3:20
- e Ne 1:9
- f Yer 32:37, 39
- g Kum 6:5
- h Mwa 12:2, 3
Yer 25:12
Omb 3:64
Ro 12:19
- i Isa 65:21, 22
Mal 3:10
- j Yer 32:37, 41
- k Ne 1:9
Mdo 3:19

sha mateka wenu^a na kuwonyesha ninyi rehema^b na kuwakusanya tena kutoka katika mataifa yote ambako Yehova Mungu wenu aliwatawanya.^c **4** Hata watu wenu wakitawanywa mpaka mwisho wa mbingu, Yehova Mungu wenu atawakusanya na kuwarudisha kutoka huko.^d **5** Yehova Mungu wenu atawarudisha katika nchi ambayo baba zenu walimiliki, nanyi mtaimiliki; naye atawafanikisha na kuwafanya mwongezeke kuliko baba zenu.^e **6** Yehova Mungu wenu ataisafisha^f mioyo yenu na mioyo ya wazao wenu,^f ili mumpende Yehova Mungu wenu kwa moyo wenu wote na kwa nafsi* yenu yote na ili muweze kuishi.^g **7** Ndipo Yehova Mungu wenu atawaletea laana hizi zote maadi wenu, waliowachukia na kuwatesa.^h

8 “Kisha mtarudi na kuisikiliza sauti ya Yehova na kushika amri zake zote ninazowaaamuru leo. **9** Yehova Mungu wenu atawaletea mafanikio mengi katika kazi yote ya mikono yenu,ⁱ atawafanya muwe na watoto wengi na mifugo mingi na mazao mengi ya ardhi yenu, kwa maana Yehova atafurahia tena kuwafanikisha, kama alivyofurahia kuwafanikisha mababu zenu.^j **10** Kwa maana wakati huo mtasikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu na kushika amri zake na sheria zilizoandikwa katika kitabu hiki cha Sheria, nanyi mtarudi kwa Yehova Mungu wenu kwa moyo wenu wote na kwa nafsi* yenu yote.^k

11 “Sasa amri hii ninayowaamuru leo si ngumu sana

30:6 #Tnn., “ataitahiri.”

kwenu, wala haiko mbali msiweze kuifikia.^a **12** Haiko mbinguni, hivi kwamba msemi, 'Ni nani atakayepanda juu mbinguni ili atuletee, tuisikie na kuishika?'^b **13** Wala haiko ng'ambo ya bahari, hivi kwamba msemi, 'Ni nani atakayevuka ng'ambo ya bahari atuletee, tuisikie na kuishika?' **14** Kwa maana neno hilo liko karibu sana nanyi, katika kinywa chenu wenyewe na katika moyo wenu wenyewe,^c ili mlitende.^d

15 "Tazameni, naweka mbele yenu leo uzima na mema, na kifo na mabaya.^e **16** Ikiwa mtazisikiliza amri za Yehova Mungu wenu ninazowaa-muru leo, kwa kumpenda Yehova Mungu wenu,^f kutembea katika njia zake, na kushika amri zake na maagizo yake na sheria zake,^{*} basi mtaiishi^g na kuongezeka, na Yehova Mungu wenu atawabariki katika nchi mnayoenda kuimiliki.^h

17 "Lakini moyo wenu ukikengeukaⁱ na kukataa kusikiliza, mshawishiwe na kuinamia miungu mingine na kuiabudu,^j **18** nawaambia ninyi leo kwamba hakika mtaangamia.^k Hamtaishi kwa muda mrefu katika nchi mnayovuka Yordani ili kuimiliki. **19** Nachukua mbingu na dunia kuwa mashahidi dhidi yenu leo kwamba nimeweka uzima na kifo mbele yenu, baraka na laana,^l nanyi lazima mchague uzima ili mwendelee kuishi,^m ninyi na wazao wenu,ⁿ **20** kwa kumpenda Yehova Mungu wenu,^o kwa kuisikiliza sauti yake, na kushikamana naye,^p kwa

30:16 *Tnn., "maamuzi yake ya hukumu."

SURA YA 30

a Isa 45:19

b Ro 10:6

c Ro 10:8

d Mt 7:21

Yak 1:25

e Kum 11:26

f Kum 6:5

g Law 18:5

h Law 25:18

Kum 30:5

i Kum 29:18

Ebr 3:12

j Kum 4:19

k Kum 8:19

Yos 23:15

1Sa 12:25

l Kum 11:26

Kum 27:26

Kum 28:2, 15

m Kum 32:47

n Yos 24:15

o Kum 10:12

p Kum 4:4

Safu ya 2

a Mwa 12:7

Mwa 15:18

SURA YA 31

b Kut 7:7

Kum 34:7

Mdo 7:23

c Hes 20:12

Kum 3:27

d Kum 9:3

e Hes 27:18

Kum 3:28

Yos 1:2

f Hes 21:23, 24

g Hes 21:33, 35

h Kut 23:23

i Hes 33:52

Kum 7:2, 24

Kum 20:16

j Yos 1:6

Zb 27:14

Zb 118:6

k Hes 14:9

Kum 7:18

l Kum 4:31

Yos 1:5

Ebr 13:5

m Yos 10:25

n Kum 1:38

o Kut 33:14

maana yeye ni uzima wenu na kwa uwezo wake mtaishi kwa muda mrefu katika nchi ambayo Yehova aliapa kwamba angewapa mababu zenu Abrahamu, Isaka, na Yakobo."^a

31 Ndipo Musa akatoka na kuwaambia Waisraeli wote maneno haya: **2** "Leo nina umri wa miaka 120.^b Siwezi tena kuwaongoza,^{*} kwa sababu Yehova ameniambia, 'Hutavuka mto huu wa Yordani.'^c **3** Yehova Mungu wenu ndiye anayevuka mbele yenu, naye mwenyewe atayaangamiza mataifa haya kutoka mbele yenu, nanyi mtayafukuza.^d Yoshua ndiye atakayewangoza kuvuka,^e kama Yehova alivyosema. **4** Yehova atayatendea kama alivyowatendea Sihoni^f na Ogu,^g wafalme wa Waamori, na nchi yao, alipowaangamiza.^h **5** Yehova atawashinda kwa niaba yenu, mtawatendea kulingana na amri yote ambayo nimewapa.ⁱ **6** Iweni jasiri na imara.^j Msiogope wala msiwe na hofu mbele yao,^k kwa sababu Yehova Mungu wenu ndiye anayepiga mwendo pamoja nanyi. Hatawatupa wala kuwaacha."^l

7 Kisha Musa akamwita Yoshua na kumwambia hivi mbele y Waisraeli wote: "Uwe jasiri na imara,^m kwa sababu ni wewe utakayewaingiza watu hawa katika nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zao kwamba atawapa, nawe utawapa iwe urithi wao.ⁿ **8** Yehova ndiye anayepiga mwendo mbele yako, naye atatendea kuwa pamoja nawe.^o

31:2 *Tnn., "kutoka nje na kuingia ndani."

Hatakutupa wala kukuacha. Usiogope wala usihofu.”^a

9 Ndipo Musa akaandika Sheria hii^b na kuwapa makuhani, Walawi, ambao wanabeba sanduku la agano la Yehova, na wazee wote wa Israeli. **10** Musa akawaamuru hivi: “Mwishoni mwa kila miaka saba, wakati uliowekwa katika mwaka wa kufuta madeni,^c wakati wa Sherehe ya Vibanda,^{*d} **11** Waisraeli wote wanapokuja mbele za Yehova^e Mungu wao mahali anapochagua, unapaswa kuisoma Sheria hii mbele ya Waisraeli wote ili waisikie.^f **12** Wakusanye watu pamoja,^g wanau-me, wanawake, watoto,^{*} na mkaaji mgeni aliye katika majiji^z yenu, ili wasikilize na kujifunza kumhusu Yehova Mungu wenu na kumwogopa yeye na kuwa waangalifu kutekeleza maneno yote ya Sheria hii. **13** Ndipo wana wao ambao hawajui Sheria hii watasikiliza^h na kujifunza kumwogopa Yehova Mungu wenu siku-zote ambazo mtaishi katika nchi ambayo mnavuka Yordani kuimiliki.”ⁱ

14 Kisha Yehova akamwambia Musa, “Tazama! Wakati wako wa kufa umekaribia,^j Mwrite Yoshua, nanyi mwende* kwenye hema la mkutano, ili nimweke yeye kuwa kiongozi.”^k Basi Musa na Yoshua wakaenda na kusimama kwenye hema la mkutano. **15** Ndipo Yehova akatokea pale hemani katika nguzo ya wingu, na nguzo hiyo ya wingu ikasimama karibu na mlango wa hema.^l

31:10 *Au “Vibanda vya Muda.” **31:12** *Tnn., “watoto wachanga.” ^zTnn., “malango.” **31:14** *Au “mchukue nafasi zenu.”

SURA YA 31

a Yos 1:9

b Kut 34:27

c Kum 15:1

d Law 23:34

e Kum 16:16

f Ne 8:7

g Kum 4:10
Ebr 10:25h Kum 6:6,7
Efe 6:4

i Kum 30:16

j Hes 27:13

k Kum 3:28

l Kut 33:9
Kut 40:38

Safu ya 2

a Amu 2:17
Zb 106:37-39

b 1Fa 11:33

c Amu 2:12, 20

d Kum 29:20

e 1Nya 28:9
2Nya 15:2
2Nya 24:20f Kum 32:20
Zb 104:29
Eze 39:23

g Ne 9:27

h Amu 6:13

i Isa 59:2

j Kum 31:30
Kum 32:44k Kum 4:9
Kum 11:19

l Kum 31:21

m Mwa 15:18

n Kut 3:8
Hes 13:26, 27

o Ne 9:25

p Kut 24:7
Kum 8:12-14
Kum 29:1
Ne 9:26

q Kum 28:59

r Kut 16:4

16 Sasa Yehova akamwambia Musa hivi: “Tazama! Unakaribia kufa,^{*} na watu hawa wataanza kufanya ukahaba wa kiroho pamoja na miungu ya kigeni inayowazunguka katika nchi wanayoenda.^a Wataniacha na kuvunja agano langu^b ambalo nimefanya pamoja nao.^c **17** Wakati huo hasira yangu itawaka dhidi yao,^d nami nitawaacha^e na kuuficha uso wangu wasiuone^f mpaka watakapoangamia. Kisha baada ya kupatwa na misiba na mateso mengi,^g watasema, ‘Je, hatujapatwa na misiba hii kwa sababu Mungu wetu hayoku miongoni mwe-tu?’^h **18** Lakini nitaendelea kuuficha uso wangu siku hiyo kwa sababu ya maovu yote waliyotenda kwa kuigeukia miungu mingine.ⁱ

19 “Sasa jandikieni wimbo huu^j na kuwafundisha Waisraeli.^k Hakikisheni kwamba wanajifunza wimbo huu* ili uwe ushahidi wangu dhidi ya Waisraeli.^l **20** Nitakapowaleta katika nchi ambayo niliwapia mababu zao^m—nchi inayotiririka maziwa na asaliⁿ—nao wale na kushiba na kufanikiwa,^{*o} wataigeukia miungu mingine na kuiabudu na kuni-dharau na kulivunja agano langu.^p **21** Watakapopatwa na misiba na mateso mengi,^q wimbo huu utakuwa ushahidi kwao (kwa sababu wazao wao hawapaswi kuusahau), kwa sababu tayari ninajua mwelekeo ambao wamesitawisha^r hata kabla sijawaingiza katika nchi niliyowaapia.”

31:16 *Tnn., “kulala na baba zako.” **31:19** *Tnn., “Utieni katika vinywa vyao.” **31:20** *Tnn., “kunepa.”

22 Basi Musa akaandika wimbo huu siku hiyo na kuwafundisha Waisraeli kuuimba.

23 Kisha akamweka* Yo-shua^a mwana wa Nuni kuwa kiongozi na kusema: "Uwe jasisiri na imara,^b kwa sababu ni wewe utakayewaingiza Waisraeli katika nchi ambayo nimewaapia,^c nami nitaendelea kuwa pamoja nawe."

24 Mara tu Musa alipomaliza kuandika maneno yote ya Sheria hii katika kitabu,^d

25 Musa akawaamuru hivi Walawi wanaobeba sanduku la agano la Yehova: 26 "Chukueni kitabu hiki cha Sheria^e mkiweke kando ya sanduku^f la agano la Yehova Mungu wenu, nacho kitakuwa ushahidi dhidi yenu mahali hapo.

27 Kwa maana mimi mwenyewe najua vizuri uasi wenu^g na ukaidi wenu.*^h Ikiwa mmekuwamkimwasi sana Yehova ningali hai pamoja nanyi, basi mtamwasi kadiri gani nikifa?

28 Nikusanyieni wazee wote wa makabila yenu na maofisa wenu, acheni niwaambie maneno haya wasikie, na acheni nichukue mbingu na dunia ziwemashahidi dhidi yao.ⁱ

29 Kwa maana najua vizuri kwamba baada ya kifo changu hakika mtatenda maovu/na kuacha njia ambayo nimewaamuru ninyi. Na bila shaka mpatatwa na msiba^k siku zijazo, kwa sababu mtatenda maovu machoni pa Yehova, nanyi mtamkasirisha kwa kazi za mikono yenu."

30 Kisha mbele ya Waisraeli wote, Musa akasema maneno ya wimbo huu kuanzia mwanzo mpaka mwisho:^l

31:23 *Inaonekana ni Mungu. 31:27 *Tnn., "shingo yenu ngumu."

SURA YA 31

a Hes 27:18
Kum 31:14

b Yos 1:6, 9

c Kum 1:38
Kum 3:28

d Kut 34:27

e Kum 17:18
2Nya 34:14

f 1Fa 8:9

g Kum 9:24
Ne 9:26

h Kut 32:9
Zb 78:8

i Kum 30:19

j Amu 2:19

k Kum 28:15

l Kum 32:44

Safu ya 2

SURA YA 32

a Yoh 17:26

b 1Nya 29:11
Zb 145:3

c 2Sa 22:31
Zb 18:2
Zb 19:7
Yak 1:17

d Zb 33:5

e Kum 7:9
1Pe 4:19

f Kum 25:16

g Mwa 18:25

h Kum 31:27
Amu 2:19
Zb 14:1

i Isa 1:4

j Zb 78:8
Lu 9:41

k Isa 1:2

l Yer 4:22

m Kut 4:22
Kum 32:18
Isa 63:16

n Kut 13:14
Zb 44:1

32 "Sikilizeni, enyi mbingu, nami nitasema, Dunia na isikie maneno ya kinywa changu.

2 Mafundisho yangu yatanyesha kama mvua; Maneno yangu yatadondoka kama umande, Kama mvua ya rasharasha juu ya majani Na kama manyunyu mengi juu ya mimea.

3 Kwa maana nitalitangaza jina la Yehova.^a Nitaongea kuhusu ukuu wa Mungu wetu!^b

4 Yeye Mwamba, kazi zake ni kamilifu,^c Kwa maana njia zake zote ni haki.^d

Mungu wa uaminifu^e ambaye kamwe hana ukosefu wa haki;^f

Yeye ni mwadilifu na mnyoofu.^g

5 Wao ndio wametenda kwa njia ya upotovu.^h

Wao si watoto wake, kasoro ni yao wenyewe.ⁱ

Wao ni kizazi kilicho komba na kilichopotoka!

6 Je, hivi ndivyo mnavyopaswa kumtendea Yehova,^k Enyi watu wajinga na wasio na hekima?^l

Je, yeye si Baba yenu ali-yewaumba,^m

Si Yeye aliyewaumba ninyi na kuwaimarisha kabisa?

7 Kumbukeni siku za zamani;

Fikirieni miaka ya vizavi vilivyopita.

Waulizeni baba zenu, nao watawaambia;ⁿ

Wazee wenu, nao watawajulisha.

- 8** Aliye Juu Zaidi alipoyapa mataifa urithi wao,^a Alipowatenganisha wana wa Adamu,^{*b} Aliweka mpaka wa mataifa^c Kulingana na idadi ya wana wa Israeli.^d
- 9** Kwa maana watu wa Yehova ni fungu lake;^e Yakobo ni urithi wake.^f
- 10** Alimpata katika nchi yenye nyika^g Na katika jangwa tupu, lenye milio.^h Alimzunguka akimlinda, akamtunza,ⁱ Na kumlinda kama mboni ya jicho lake.^j
- 11** Kama tai anavyokitikisa kiota chake, Anavyopaa juu ya makinda yake, Akitandaza mabawa yake, na kuwachukua, Akiwabeba juu ya mabawa yake,^k
- 12** Yehova peke yake aliendelea kumwongoza;^{*l} Hakuna mungu yeyote wa kigeni aliyekuwa pamoja naye.^m
- 13** Alimpitisha juu ya sehemu za juu za dunia,ⁿ Hivi kwamba akala mazao ya shambani.^o Alimlisha asali kutoka katika jabali Na mafuta kutoka katika mwamba mgumu,
- 14** Siagi ya mifugo na maziwa ya kundi, Pamoja na kondoo bora,^{*} Na kondoo dume wa Bashani, na mbuzi dume,

32:8 *Au labda, "Alipoitenganisha jamii ya wanadamu." 32:12 *Yaani, Yakobo. 32:14 *Tnn., "mafuta ya kondoo."

SURA YA 32

a Mwa 10:5
Zb 115:16

b Mwa 11:9

c Kum 2:5, 19
Mdo 17:26

d Mwa 15:18
Kut 23:31

e Kut 19:5
Kum 7:6

f Zb 78:71

g Kum 8:14, 15

h Yer 2:6

i Ne 9:19, 20

j Zek 2:8

k Kut 19:4

l Kum 1:31

m Isa 43:12

n Kum 33:29

o Kum 8:7, 8

Safu ya 2

a Zb 147:14

b Kum 31:20
Ne 9:25

c Isa 1:4
Ho 13:6

d Amu 2:12
1Fa 14:22
1Ko 10:21, 22

e 2Fa 23:13
Eze 8:17

f Law 17:7
Zb 106:37
1Ko 10:20

g Zb 106:21
Isa 17:10
Yer 2:32

h Kum 4:34

i Amu 2:14
Zb 78:59

j Kum 31:17

k Kum 32:5
Isa 65:2
Mt 17:17

l Isa 1:2

Pamoja na ngano bora;^{*a} Nawe ulikunywa divai kutoka katika damu[#] ya zabibu.

- 15** Yeshuruni* aliponenepa, alipiga teke kwa uasi. Umenepa, una mafuta mengi mwilini, tumbo lako limenenepa.^b Basi akamwacha Mungu, aliyemuumba,^c Na kumdharau Mwamba wa wokovu wake.
- 16** Kwa miungu ya kigeni walichochea hasira yake kali;^d Walikuwa wakimkasirisha kwa mambo yanayochukiza.^e
- 17** Walikuwa wakiwatolea dhahihu roho waovu, wala si Mungu,^f Miungu ambayo hawakuijua, Mipya iliyokuja hivi karibuni, Miungu ambayo mababu zenu hawakuijua.
- 18** Mlimsahau Mwamba,^g baba yenu aliyewazaa, Nanyi hamkumkumbuka Mungu aliyewazaa.^h
- 19** Yehova alipoona hilo, aliwakataaⁱ Kwa sababu wanawe na mabinti zake walimkasirisha.
- 20** Kwa hiyo akasema, 'Nitauficha uso wangu wasiuone;^j Nitaona kitakachowapata. Kwa maana wao ni kizazi kilichopotoka,^k Wana ambao hawana uaminifu.^l

32:14 *Tnn., "mafuta ya figo ya ngano." #Au "maji." 32:15 *Maana yake "Mnyoofu," jina la heshima la Israeli.

- 21** Wamechochea hasira yangu kali* kwa kitu ambacho si mungu;^a
Wamenikasirisha kwa sanamu zao za ubatili.^b
Kwa hiyo nitawachochea wawe na wivu kwa wale ambao si taifa;^c
Nitawakasirisha kwa kutumia taifa lenye ujinga.^d
- 22** Kwa maana hasira yangu imewasha moto^e
Ambao utateketeza mpaka kwenye kina cha Kaburi,^{*f}
Nao utateketeza dunia na mazao yake
Na kuchoma moto misingi ya milima.
- 23** Nitazidisha misiba yao;
Nitawapiga kwa mishale yangu mpaka iishe.
- 24** Watachoka kwa sababu ya njaa^g
Na kuliwa na homa kali na maangamizi machungu.^h
Nitawatumia meno ya wanyama ili yawashambulieⁱ
Na sumu ya wanyama wa-naotambaa mavumbini.
- 25** Nje, upanga utawaangamiza watoto wao;^j
Na ndani, kuna hofu^k
Kwa kijana na bikira,
Mtoto anayenyonya pamoja na mzee mwenye mvi.^l
- 26** Ningesema: "Nitawatawanya;
Nitafanya ukumbusho wao usahauliwe kabisa miongoni mwa wanadamu,"
- 27** Ingingekuwa kwa sababu ya kuogopa jinsi maadui wangu watakvoyotenda,^m

32:21 *Au "wivu wangu." 32:22 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 32

- a Zb 96:5
1Ko 10:21, 22
- b 1Sa 12:10, 21
- c Ho 2:23
Ro 9:25
Ro 11:11
1Pe 2:10
- d Ro 10:19
- e Omb 4:11
- f Amo 9:2
- g Kum 28:53
- h Kum 28:21, 22
- i Law 26:22
- j Omb 1:20
- k Eze 7:15
- l 2Nya 36:17
Omb 2:21
- m 1Sa 12:22
Eze 20:14

Safu ya 2

- a Kut 32:12
Hes 14:15, 16
- b Zb 115:2
- c Mt 13:15
- d Zb 81:13
- e Ho 14:9
- f Yer 2:19
- g 2Nya 24:24
- h Amu 2:14
1Sa 12:9
- i 1Sa 2:2
- j Kut 14:25
1Sa 4:8
Ezr 1:2, 3
- k Yud 7
- l Isa 5:4
Yer 2:21
- m Ro 2:5
- n Nah 1:2
Ro 12:19
Ebr 10:30
- o Zb 73:12, 18

- Kwa sababu huenda wapi-nzani wakalielewa vibaya jambo hilo.^a
Huenda wakasema: "Nguvu zetu zimeshinda;^b
Si Yehova aliyefanya mambo haya yote."
- 28** Kwa maana wao ni taifa lisilo na akili,^{*}
Na hawana uelewaji miongoni mwao.^c
- 29** Laiti wangukuwa na hekima!^d Wangetafakari jambo hili.^e
Wangefikiria mwisho wao.^f
- 30** Mtu mmoja angewezaje kuwakimbiza 1,000,
Na wawili kuwafanya 10,000 wakimbie?^g
Kama Mwamba wao hangekuwa amewauza^h
Na Yehova kuwatia mikononi mwa maadui?
- 31** Kwa maana mwamba wao si kama Mwamba wetu,ⁱ
Hata maadui wetu wamelewa hilo.^j
- 32** Kwa maana mzabibu wao unatoka katika mzabibu wa Sodoma
Na kutoka katika matuta ya Gomora.^k
Zabibu zao ni zabibu za sumu,
Vishada vyao ni vichungu.^l
- 33** Divai yao ni sumu ya nyoka,
Sumu kali ya swila.
- 34** Je, hili sijaliweka akibani,
Na kulifungia kabisa katika ghala langu?^m
- 35** Kisasi ni changu, na malipo,ⁿ
Wakati utakapofika ambapo mguu wao utateleza,^o
Kwa maana siku ya msiba wao iko karibu,

32:28 *Au labda, "lisilosikia ushauri."

- Na kinachowasubiri kitafika haraka.’
- 36** Kwa maana Yehova atawahukumu watu wake,^a Naye atawahurumia* watumishi wake^b Atakapoona nguvu zao zimeisha, Na kwamba waliobaki ni wasio na uwezo na walio dhaifu peke yao.
- 37** Ndipo atakaposema, ‘Muingu yao iko wapi,^c Mwamba ambao waliukimibia,
- 38** Iliyokuwa ikila mafuta ya dhabihu zao,* Na kunywa divai ya matoleo yao ya kinywaji?^d Acheni iinuke na kuwasaidia ninyi. Na iwe kimbilio lenu.
- 39** Sasa tazameni kwamba mimi—mimi ndiye,^e Na hakuna miungu mingine ila mimi.^f Mimi huua, nami hufanya kuwa hai.^g Ninajeruhi,^h nami nita-ponya,ⁱ Na hakuna anayeweza kumwokoia yeyote kutoka mikononi mwangu.^j
- 40** Kwa maana nainua mkono wangu mbinguni, Na kuapa hivi: “Kwa hakika kama niishivyo milele,”^k
- 41** Nikiunoa upanga wangu unaometameta Na kuutayarisha mkono wangu ili uhukumu,^l Nitawalipiza kisasi maadui wangu^m Na kuwalipa wale wanaonichukia.

32:36 *Au “ataghairi kwa sababu ya.”
32:38 *Au “kula dhabihu zao bora.”

SURA YA 32

a Ebr 10:30

b Amu 2:18
Zb 90:13
Zb 106:45
Zb 135:14

c Amu 10:14

d Ho 2:8
1Ko 10:20, 21e Isa 41:4
Isa 48:12

f Kum 4:35

g 1Sa 2:6
Zb 68:20

h 2Nya 21:16, 18

i Hes 12:13
Yer 17:14

j Isa 43:13

k 1Ti 1:17
Ufu 10:5, 6

l Nah 1:3

m Isa 1:24
Isa 59:18

Safu ya 2

a Mwa 12:2, 3
1Fa 8:43
Ro 3:29
Ro 15:10b 2Fa 9:7
Ufu 6:10

c Mik 5:15

d Ufu 15:3

e Hes 11:28
Kum 31:22, 23

f Kum 11:18

g Kum 6:6, 7

h Law 18:5
Kum 30:19
Ro 10:5

i Hes 27:12

j Kum 34:1

k Mwa 10:19
Mwa 15:18
Yos 1:3

42 Nitailewesha mishale yangu kwa damu, Na upanga wangu utakula nyama, Pamoja na damu ya waliouawa na pia mateka, Pamoja na vichwa vya viongozi wa adui.’

43 Furahini, enyi mataifa, pamoja na watu wake,^a Kwa maana atailipizia kisasi damu ya watumishi wake,^b Atawalipiza kisasi maadui wake^c Na kufunika dhambi ya* nchi ya watu wake.”

44 Basi Musa akaja na ku- yasema maneno yote ya wimbo huo watu wakisikia;^d alikuwa na Hoshea*^e mwana wa Nuni. **45** Musa alipomaliza kuwaambia Waisraeli wote maneno hayo yote, **46** aka- waambia hivi: “Wekeni mio- yoni mwenu maonyo yote ni- liyowapa leo,^f ili muwaamu- ru wana wenu wawe waanga- lifu kutenda maneno yote ya Sheria hii.^g **47** Kwa maana haya si maneno matupu kwe- nu, bali yanamaanisha uhai wenu,^h na kwa maneno haya mnaweza kuishi kwa muda mrefu katika nchi ambayo mnavuka Yordani kuimiliki.”

48 Yehova akaongea na Musa siku hiyohiyo na kumwa- mbia hivi: **49** “Panda juu ya mlima huu wa Abarimu,ⁱ Mli- ma Nebo,^j ulio katika nchi ya Moabu, unaoelekeana na Yeri- ko, nawe utazame nchi ya Ka- naani, ninayowapa Waisraeli waimiliki.^k **50** Kisha utaku-

32:43 *Au “Na kuisafisha.” 32:44 *Jina la awali la Yoshua. Hoshea ni ufu- pisho wa jina Hoshaya, linalomaanisha “Aliyeokolewa na Yah; Yah Ameokoa.”

fa juu ya mlima utakaopanda hivi punde, na kuzikwa pamoja na watu wako,* kama Haruni ndugu yako alivyokufa juu ya Mlima Hori^a na kuzikwa pamoja na watu wake, **51** kwa sababu nyote wawili hamkuwa waaminifu kwangu miongoni mwa Waisraeli kwenye maji ya Meriba^b kule Kadeshi katika nyika ya Zini, kwa sababu hamkunitakasa mbele ya Waisraeli.^c **52** Utaiona nchi hiyo kwa mbali, lakini hutaingia katika nchi hiyo ninayowapa Waisraeli.”^d

33 Sasa hii ndiyo baraka ambayo Musa mtu wa Mungu wa kweli aliwatangazia Waisraeli kabla ya kifo chake.^e
2 Alisema hivi:

“Yehova—alikuja kutoka Sinai,^f

Naye akawaangazia kutoka Seiri.

Aliangaza kwa utukufu kutoka katika eneo lenye milima la Parani,^g

Naye alikuwa pamoja na makumi ya maelfu ya watakatifu,^h

Na mashujaa wake kwenye mkono wake wa kuume.ⁱ

3 Aliwapenda watu wake;^j
 Watakatifu wao wote wako mikononi mwako.^k
 Waliketi miguuni pako;^l
 Walianza kusikiliza maneno yako.^m

4 (Musa alitupatia amri, sheria,ⁿ
 Kuwa miliki ya kutaniko la Yakobo.)^o

5 Naye akawa mfalme kule Yeshuruni,^{*p}

32:50 *Tnn., “kukusanywa kwa watu wako.” Huu ni msemu wa kishairi unao-rejelea kifo. **33:5** *Maana yake “Mnyoofu,” jina la heshima la Israeli.

SURA YA 32

a Hes 20:28

Hes 33:38

b Hes 20:12, 13

c Law 22:32

Isa 8:13

d Hes 27:13, 14

Kum 3:27

Kum 34:4, 5

SURA YA 33

e Mwa 49:28

f Kut 19:18

g Hab 3:3

h Da 7:10

Yud 14

i Zb 68:17

j Kum 7:8

Ho 11:1

k Kut 19:6

l Kut 19:23

m Kut 20:19

n Kut 24:8

o Kum 4:8

Mdo 7:53

p Isa 44:2

Safu ya 2

a Kut 18:25

Kut 19:7

b Hes 1:44, 46

c Mwa 49:3

d Hes 26:7

Yos 13:15

e Mwa 49:8

1Nya 5:2

f Zb 78:68

g Amu 1:2

2Sa 7:8, 9

h Mwa 49:5

Hes 3:12

i Kut 28:30

Law 8:6, 8

j Kut 32:26

k Kut 17:7

l Hes 20:13

m Kut 32:27

Law 10:6, 7

n Mal 2:4, 5

o Kum 17:9

p 2Nya 17:8, 9

Mal 2:7

q Kut 30:7

Hes 16:40

Viongozi wa watu walipokusanyika pamoja,^a

Pamoja na makabila yote ya Israeli.^b

6 Rubeni na aishi wala asife,^c

Na watu wake wasiwe wachache.”^d

7 Naye akamtangazia Yuda baraka hii:^e

“Ee Yehova, isikie sauti ya Yuda,^f

Nawe umrudishe kwa watu wake.

Mikono yake imetetea* kilicho chake,

Nawe umsaidie dhidi ya maadui wake.”^g

8 Akasema hivi kumhusu Lawi:^h

“Thumimu yako* na Uri-muⁱ yako ni vya mtu aliye mshikamanifu kwako,^j

Uliyemjaribu kule Masa.^k

Ulianza kupambana naye karibu na maji ya Meriba,^l

9 Mtu aliyemwambia baba yake na mama yake, ‘Sijawaheshimu.’

Hata ndugu zake hakuwatabua,^m

Na watoto wake mwenyewe aliwapuza.

Kwa maana walitii neno lako,

Na kulishika agano lako.ⁿ

10 Acha wamfundishe Yakobo amri zako*^o

Na Waisraeli Sheria yako.^p

Acha wakufukizie uvumba wenye harufu inayokupendeza*^q

33:7 *Au “imepigania.” **33:8** *Neno “yako” katika mstari huu linamrejelea Mungu. **33:10** *Tnn., “maamuzi yako ya hukumu.” *Tnn., “inayopendeza pua ni mwako.”

- Na dhabihu nzima ya kuteketezwa kwenye madhabu yako.^a
- 11** Ee Yehova, bariki nguvu zake, Na ufurahie kazi ya miko-no yake. Ivunje miguu ya* wale wanaoinuka dhidi yake, Ili wale wanaomchukia wasiinuke tena.”
- 12** Alisema hivi kumhusu Benjamini:^b “Mwache mpendwa wa Yehova akae kwa usalama kando yake; Akimkinga siku nzima, Atakaa katikati ya mabega yake.”
- 13** Alisema hivi kumhusu Yosefu:^c “Nchi yake na ibarikiwe na Yehova^d Kwa vitu bora vya mbinguni, Kwa umande na maji kutoka katika chemchemi zilizo chini.^e
- 14** Kwa vitu bora vinavyole-twa na jua Na mazao bora kila mwezi,^f
- 15** Kwa vitu bora kabisa kutoka katika milima ya zamani^{*g} Na vitu bora kutoka katika vilima vinavyodumu,
- 16** Kwa vitu bora vya dunia na vitu vinavyoijaza,^h Na kwa kibali cha Yule anayekaa katika kichaka cha miiba.ⁱ Na vije juu ya kichwa cha Yosefu, Juu ya utosi wa kichwa

SURA YA 33

a Law 1:9

b Mwa 49:27

c Mwa 49:22

d Yos 16:1

e Mwa 49:25

f Law 26:5
Zb 65:9

g Yos 17:17, 18

h Kum 8:7, 8

i Kut 3:4
Mdo 7:30

Safu ya 2

a Mwa 37:7
Mwa 49:26
1Nya 5:1, 2

b Mwa 48:19, 20

c Mwa 49:13

d Mwa 49:14

e Mwa 49:19

f Yos 13:24-28

g Hes 32:1-5

h Yos 22:1, 4

cha yule aliyechaguliwa kutoka kati ya ndugu zake.^a

- 17** Fahari yake ni kama ya mzaliwa wa kwanza wa ng'ombe dume, Na pembe zake ni pembe za fahali mwitu. Atazitumia kuyasukuma* mataifa Yote pamoja mpaka miisho ya dunia. Wao ni makumi ya maelfu ya Efraimu,^b Nao ni maelfu ya Manase.”
- 18** Alisema hivi kumhusu Zabuloni:^c

“Shangilia, Ee Zabuloni, unapotoka nje, Nawe, Isakari, katika mahema yako.^d

- 19** Watayaita mataifa mli-mani. Huko watatoa dhabihu za uadilifu. Kwa maana watafyonza* utajiri mwingi wa bahari Na marundo yaliyofichika[#] mchangani.”
- 20** Alisema hivi kumhusu Gadi:^e

“Amebarikiwa yule anayepanua mipaka ya Gadi.^f Analala huko kama simba, Akiwa tayari kuunyafua mkono, naam, utosi wa kichwa.

- 21** Atajichagulia fungu la kwanza,^g Kwa maana huko fungu la mpaji sheria limehifadhwi.^h Viongozi wa watu watakusanyika pamoja.

33:17 *Au “kuyapiga.” 33:19 *Tnn., “watanyonya.” #Au “hazina zilizofichika.”

33:11 *Au “Vivunje viuno vya.” 33:15 *Au labda, “milima ya mashariki.”

Uadilifu wa Yehova ataute-
keleza,
Na amri zake* pamoja na
Israeli.”

22 Alisema hivi kumhusu
Dani:^a

“Dani ni mwanasimba.^b
Ataruka kutoka Bashani.”^c

23 Alisema hivi kumhusu
Naftali:^d

“Naftali ameshiba kibali
Naye amejaa baraka ya
Yehova.

Imiliki magharibi na ku-
sini.”

24 Alisema hivi kumhusu
Asheri:^e

“Asheri amebarikiwa kuwa
na wana.

Na apendwe na ndugu
zake,

Naye aachoye* miguu yake
katika mafuta.

25 Makufuli ya lango lako ni
chuma na shaba,^f

Nawe utakuwa salama siku
zako zote.*

26 Hakuna aliye kama Mungu
wa kweli^g wa Yeshuruni,^h

Anayepita mbinguni kuja
kukusaidia

Na kupita juu ya mawingu
katika fahari yake.ⁱ

27 Mungu ni kimbilio tangu
nyakati za kale,^j

Mikono yake ya milele iko
chini yako.^k

Naye atamfukuza adui ku-
toka mbele yako,^l

Naye atasema, ‘Waanga-
mize!’^m

28 Israeli atakaa kwa usa-
lama,

33:21 *Tnn., “maamuzi yake ya hu-
kumu.” **33:24** *Au “anawe.” **33:25**
*Tnn., “Kama zilivyo siku zako ndivyo zi-
takavyokuwa nguvu zako.”

SURA YA 33

a Mwa 49:16

b Amu 13:2, 24
Amu 15:8, 20
Amu 16:30

c Yos 19:47

d Mwa 49:21

e Mwa 49:20

f Kum 8:7, 9

g Kut 15:11

h Isa 44:2

i Zb 68:32-34

j Zb 46:11

Zb 91:2

k Isa 40:11

l Kum 9:3

m Kum 31:3, 4

Safu ya 2

a Kum 8:7, 8

b Kum 11:11

c Zb 33:12
Zb 144:15
Zb 146:5

d Kum 4:7
2Sa 7:23
Zb 147:20

e Zb 27:1
Isa 12:2

f Zb 115:9

g Zb 66:3

SURA YA 34

h Kum 32:49

i Kum 3:27

j Hes 36:13

k Amu 18:29

l Kut 23:31
Hes 34:2, 6
Kum 11:24

m Yos 15:1

n Mwa 13:10

o Mwa 19:22, 23

p Mwa 12:7
Mwa 26:3
Mwa 28:13

q Hes 20:12

Na chemchemi ya Yakobo
itatengwa peke yake

Katika nchi ya nafaka na
divai mpya,^a

Na anga lake litadondosha
umande.^b

29 Wewe ni mwenye furaha,
Ee Israeli!^c

Ni nani aliye kama wewe,^d
Taifa linalofurahia woko-
vu wa Yehova,^e

Ngao yenu inayowalinda^f
Na upanga wenu wenye
fahari?

Maadui wenu watajikunya-
ta mbele yenu,^g

Nanyi mtawakanyaga mi-
gongoni.”*^h

34 Kisha Musa akatoka ka-
tika jangwa tambarare
la Moabu na kupanda Mlima
Nebo,^h kwenye kilele cha Pis-
ga,ⁱ kinachoelekeana na Ye-
riko.^j Yehova akamwonye-
sha nchi yote, kuanzia Gileadi
mpaka Dani,^k **2** na nchi yote
ya Naftali na nchi ya Efrai-
mu na Manase, na nchi
yote ya Yuda mpaka bahari
ya magharibi,^l **3** na Nege-
bu^m na ile Wilaya,ⁿ bonde ta-
mbarare la Yeriko, jiji la mite-
nde, mpaka Soari.^o

4 Kisha Yehova akamwa-
mbia hivi: “Hii ndiyo nchi
ambayo nilimwambia Abraha-
mu, Isaka, na Yakobo, nilipo-
sema, ‘Nitaupa uzao wako*
nchi hii.’^p Nimekuruhusu uio-
ne kwa macho yako mwenye-
we, lakini hutavuka kuingia
humo.”^q

5 Kisha Musa mtumishi
wa Yehova akafa huko kati-
ka nchi ya Moabu kama

33:29 *Au labda, “mtakanyaga maha-
li pao pa juu.” **34:2** *Yaani, ile Bahari
Kuu, Mediterania. **34:4** *Tnn., “Nitaipa
mbegu yako.”

Yehova alivyosema.^a **6** Akamzika bondeni katika nchi ya Moabu, ng'ambo ya Bethpeori, na hakuna mtu anayejua kaburi lake liko wapi mpaaka leo hii.^b **7** Musa alikuwa na umri wa miaka 120 alipokufa.^c Macho yake hayakuwa yamedhoofika, na nguvu zake hazikuwa zimeisha. **8** Waisraeli walimlilia Musa katika jangwa tamarare la Moabu kwa siku 30.^d Kisha siku za kumlilia na kumwbolezea Musa zikaisha.

9 Yoshua mwana wa Nuni alikuwa amejaa roho ya hekima, kwa kuwa Musa aliku-

SURA YA 34

a Kum 32:50

Yos 1:2

b Yud 9

c Kum 31:1, 2

Mdo 7:23

Mdo 7:30, 36

d Hes 20:29

Safu ya 2

a Kum 31:14

ITI 4:14

b Hes 27:18, 21

Yos 1:16

c Kum 18:15

Mdo 3:22

Mdo 7:37

d Kut 33:11

Hes 12:8

e Kum 4:34

f Kum 26:8

Lu 24:19

wa ameweka mkono wake juu yake;^a na Waisraeli wakaanza kumsikiliza, nao wakafanya kama Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.^b **10** Lakini hajatokea tena nabii mwingine katika Israeli aliye kama Musa,^c ambaye Yehova alimjua uso kwa uso.^d **11** Alifanya ishara zote na miujiza ambayo Yehova alimtuma afanye katika nchi ya Misri kwa Farao na watumishi wake wote na nchi yake yote,^e **12** pamoja na mkono wenye nguvu na nguvu zinazoogopesha ambazo Musa alidhihirisha machoni pa Waisraeli wote.^f

YOSHUA

YALIYOMO

- | | |
|---|---|
| <p>1 Yehova amtia moyo Yoshua (1-9)
Soma Sheria kwa sauti ya chini (8)
Matayarisho ya kuvuka Yordani (10-18)</p> <p>2 Yoshua atuma wapelelezi wawili
Yeriko (1-3)
Rahabu awaficha wapelelezi (4-7)
Rahabu apewa ahadi (8-21a)
Ishara ya kamba nyekundu (18)
Wapelelezi warudi kwa Yoshua (21b-24)</p> <p>3 Waisraeli wavuka Yordani (1-17)</p> <p>4 Mawe ya ukumbusho (1-24)</p> <p>5 Waisraeli watahiriwa kule Gilgali (1-9)
Sherehe ya Pasaka; mwisho wa mana (10-12)
Mkuu wa jeshi la Yehova (13-15)</p> <p>6 Kuta za Yeriko zaanguka (1-21)
Rahabu na familia yake waokolewa (22-27)</p> <p>7 Waisraeli washindwa kule Ai (1-5)
Sala ya Yoshua (6-9)
Dhambi yasababisha Waisraeli washindwe (10-15)</p> | <p>Akani afichuliwa na kupigwa mawe (16-26)</p> <p>8 Yoshua avamia Ai (1-13)
Jiji la Ai latekwa (14-29)
Sheria yasomwa kwenye Mlima Ebali (30-35)</p> <p>9 Wagibeoni wajanja watafuta amani (1-15)
Hila ya Wagibeoni yagunduliwa (16-21)
Wagibeoni watakuwa watekaji wa maji na wakusanyaji wa kuni (22-27)</p> <p>10 Waisraeli wawatetea Wagibeoni (1-7)
Yehova awapigania Waisraeli (8-15)
Mawe yawaangukia maadui wanaokimbia (11)
Jua lasimama tuli (12-14)
Wafalme watano wa maadui wauawa (16-28)
Majiji ya kusini yatekwa (29-43)</p> <p>11 Majiji ya kaskazini yatekwa (1-15)
Muhtasari wa ushindi wa Yoshua (16-23)</p> <p>12 Wafalme wa mashariki mwa Yordani washindwa (1-6)</p> |
|---|---|

- Wafalme wa magharibi mwa Yordani washindwa (7-24)
- 13 Maeneo ambayo hayajatekwa (1-7)
Kugawanywa kwa maeneo mashariki mwa Yordani (8-14)
Urithi wa kabila la Rubeni (15-23)
Urithi wa kabila la Gadi (24-28)
Urithi wa kabila la Manase upande wa mashariki (29-32)
Yehova ni urithi wa Walawi (33)
- 14 Kugawanywa kwa maeneo magharibi mwa Yordani (1-5)
Kalebu arithi Hebroni (6-15)
- 15 Urithi wa kabila la Yuda (1-12)
Binti ya Kalebu apewa eneo (13-19)
Majiji ya Yuda (20-63)
- 16 Urithi wa wazao wa Yosefu (1-4)
Urithi wa kabila la Efraimu (5-10)
- 17 Urithi wa kabila la Manase upande wa magharibi (1-13)
Maeneo zaidi kwa ajili ya wazao wa Yosefu (14-18)
- 18 Maeneo yaliyobaki yagawanywa huko Shilo (1-10)
Urithi wa kabila la Benjamini (11-28)
- 19 Urithi wa kabila la Simeoni (1-9)
Urithi wa kabila la Zabuloni (10-16)
Urithi wa kabila la Isakari (17-23)
Urithi wa kabila la Asheri (24-31)
- Urithi wa kabila la Naftali (32-39)
Urithi wa kabila la Dani (40-48)
Urithi wa Yohua (49-51)
- 20 Majiji ya makimbilio (1-9)
- 21 Majiji ya Walawi (1-42)
Ya wazao wa Haruni (9-19)
Ya Wakohathi waliobaki (20-26)
Ya Wagershoni (27-33)
Ya Wamerari (34-40)
Ahadi za Yehova zatimia (43-45)
- 22 Makabila ya mashariki yarudi nyumbani (1-8)
Madhabahu yajengwa karibu na Yordani (9-12)
Kusudi la madhabahu laelezwa (13-29)
Mgogoro wasuluhishwa (30-34)
- 23 Maneno ya mwisho ya Yohua kwa viongozi wa Waisraeli (1-16)
Hakuna ahadi yoyote ya Yehova iliyokosa kutimia (14)
- 24 Yohua awakumbusha Waisraeli historia yao (1-13)
Awahimiza wamtumikie Yehova (14-24)
"Mimi na familia yangu, tutamtumikia Yehova" (15)
Yohua afanya agano na Waisraeli (25-28)
Yohua afa na kuzikwa (29-31)
Mifupa ya Yosefu yazikwa Shekemu (32)
Elezari afa na kuzikwa (33)

1 Baada ya kifo cha Musa mtumishi wa Yehova, Yehova akamwambia Yohua*^a mwana wa Nuni, mhudumu^b wa Musa: **2** "Musa mtumishi wangu amekufa.^c Sasa jitayarishe, vuka Mto Yordani pamoja na watu hawa wote, mwingie katika nchi ambayo ninawapa Waisraeli.^d **3** Nita-wapa kila mahali mtakapokanyaga, kama nilivyomwahidi Musa.^e **4** Eneo lenu litaanzia

1:1 *Au "Yehoshua," maana yake "Yehova Ni Wokovu."

SURA YA 1

- a Kum 31:14
b Kut 24:13
Hes 11:28
c Kum 34:5
d Kum 3:28
e Kum 11:24

Safu ya 2

- a Hes 13:29
b Mwa 15:18
Kut 23:31
Hes 34:2, 3
Kum 1:7
Yos 15:1, 4
c Kum 7:24
Kum 11:25
d Kut 3:12
Yos 3:7
e Kum 31:6
f Kum 31:23

nyikani mpaka kwenye Mlima Lebanoni hadi ule mto mku-bwa, Efrati, yaani, nchi yote ya Wahiti,^a mpaka kwenye Bahari Kuu,^b upande wa magharibi.^{#b} **5** Hakuna yeyote atakayekushinda sikuzote za masha yako.^c Nitakuwa pamoja nawe kama nilivyokuwa pamoja na Musa.^d Sitakutupa wala kukuacha.^e **6** Uwe jasiri na imara,^f kwa sababu ni wewe utakayewaongoza watu hawa

1:4 *Yaani, Mediterania. [#]Au "kuelekea machweo ya jua."

kuirithi nchi niliyowaapia mababu zao kwamba nitawapa.^a

7 “Ila tu uwe jasiri na imara kabisa, na ufuate kwa uangalifu Sheria yote kama Musa mtumishi wangu alivyokuamuru. Usiende kushoto wala kulia,^b ili utende kwa hekima mahali popote utakapoenda.^c **8** Kitabu hiki cha Sheria kisiondoke kinywani mwako,^d ni lazima ukisome kwa sauti ya chini* mchana na usiku ili ufuate kwa uangalifu mambo yote yaliyoandikwa humo;^e ndipo utakapofanikisha njia yako na kutenda kwa hekima.^f **9** Je, si mimi niliyekuamuru uwe jasiri na imara? Basi uwe jasiri na imara. Usitetemeke wala kuogopa, kwa maana mimi Yehova Mungu wako nipo pamoja nawe mahali popote utakapoenda.”^g

10 Ndipo Yoshua akawaamuru viongozi wa watu akisema, **11** “Piteni katika kambi yote na kuwaamuru watu hivi: ‘Tayarisheni vyakula, kwa sababu baada ya siku tatu mtavuka Mto Yordani ili kuingia na kuimiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa.’”^h

12 Kisha Yoshua akawaambia hivi watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase: **13** “Kumbukeni amri ambayo Musa mtumishi wa Yehova aliwapa aliposema,ⁱ ‘Yehova Mungu wenu anawapumzisha, naye amewapa nchi hii. **14** Wake zenu, watoto wenu, na wanyama wenu wa kufugwa watakaa katika nchi ambayo Musa amewapa upande huu* wa Yordani,^j lakini ninyi nyote mashujaa ho-

1:8 *Au “ukitafakari.” 1:14 *Yaani, upande wa mashariki.

SURA YA 1

a Mwa 12:7
Mwa 15:18
Mwa 26:3

b Kum 5:32

c Kum 29:9
1Fa 2:3

d Kum 6:6
Kum 30:14

e Kum 17:18, 19
Zb 1:1, 2
ITI 4:15
Yak 1:25

f 1Nya 22:13

g Kut 23:27
Kum 31:7, 8

h Kum 9:1
Yos 3:2, 3

i Hes 32:20-22
Yos 22:1-4

j Kum 3:19, 20
Kum 29:8
Yos 13:8

Safu ya 2

a Hes 1:3
Hes 26:2

b Kum 3:18

c Hes 32:33
Yos 22:4, 9

d Hes 32:17, 25

e Hes 27:18, 20
Kum 34:9

f Kum 17:12

g Kum 31:7
Yos 1:6, 9

SURA YA 2

h Hes 25:1
Hes 33:49

i Yos 6:17
Mt 1:5
Ebr 11:31
Yak 2:25

dari^a mnapaswa kuvuka na kuwatangulia ndugu zenu mkiwa mmejipanga kivita.^b Mnapaswa kuwasaidia **15** mpaka Yehova atakapowapa ndugu zenu mahali pa kupumzika, kama alivyowapa ninyi, nao pia wamiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa. Kisha rudini na kuimiliki nchi yenu ambayo Musa mtumishi wa Yehova aliwapa upande wa mashariki wa Yordani.”^c

16 Wakamwambia Yoshua: “Tutafanya yote ambayo umeutumuru, na tutaenda mahali popote unapotaka twende.^d **17** Kama tulivyomtii Musa katika mambo yote, ndivyo tutakavyokutii. Yehova Mungu wako na awe pamoja nawe kama alivyokuwa pamoja na Musa.^e **18** Mtu yeyote atakayeasi agizo lako na asiyeti amri yoyote utakayotoa atauawa.^f Lakini uwe jasiri na imara.”^g

2 Kisha Yoshua mwana wa Nuni akawatuma kwa siri wanaume wawili wapelelezi kutoka Shitimu,^h akawaambia: “Nendeni mkaipeleleze nchi, hasa jiji la Yeriko.” Basi wakaenda na kufika nyumbani kwa mwanamke mmoja kababa aliyetitwa Rahabu,ⁱ wakaaka humo. **2** Mfalme wa Yeriko akaambiwa: “Wanaume Waisraeli wameingia humu leo usiku ili kuipeleleza nchi.” **3** Ndipo mfalme wa Yeriko akawatuma wajumbe kwa Rahabu, akisema: “Watoe nje wanaume waliokuja nyumbani mwako, kwa sababu wamekuja kuipeleleza nchi nzima.”

4 Lakini mwanamke huyo alikuwa amewaficha wanauume hao wawili. Basi akase-

ma: "Ni kweli, wanaume hao walikuja kwangu, lakini siku-jua walikotoka. **5** Giza lili-poingia, waliondoka kabla ya lango la jiji kufungwa. Sijui walikokwenda, mkiwafuatia haraka, mtawafikia." **6** (Lakini alikuwa amewaficha juu ya paa katikati ya majani ya kitani yaliyopangwa paani.) **7** Basi watu hao wakawafuatia kwenye vivuko vya Yordani,^a na mara tu walipotoka, lango la jiji likafungwa.

8 Kabla wapelelezi hao hawajalala, Rahabu akaenda kuwaona kwenye paa. **9** Akawaambia: "Najua kwamba Yehova atawapa nchi hii^b na tumeshikwa na hofu kwa sababu yenu.^c Wakaaji wote wa nchi wamevunjika moyo kwa sababu yenu,^d **10** kwa maana tumesikia jinsi Yehova alivyoyakausha maji ya Bahari Nyekundu* mbele yenu mlipotoka Misiri^e na mambo mliyowatendea wale wafalme wawili wa Waamori, yaani, Sihoni^f na Ogu,^g waliokuwa ng'ambo ya^h Yordani, mliowaangamiza kabisa. **11** Tuliposikia hayo, tulikufa moyo,* na hakuna yeyote aliye na ujasiri kwa sababu yenu, kwa kuwa Yehova Mungu wenu ni Mungu juu mbinguni na chini duniani.^h **12** Sasa, tafadhalini, niapieni kwa Yehova kwamba, kwa kuwa nimewatendea kwa upendo mshikamanifu, ninyi pia mtaitendea familia ya baba yangu kwa upendo mshikamanifu; nipeni ishara inayoaminika* kwamba mtatimiza ahadi yenu. **13** Nanyi hamtawaa-

2:10 *Au "Bahari ya Shamu." ^aYaani, upande wa mashariki wa. 2:11 *Tnn., "mioyo yetu iliyeyuka." 2:12 *Au "inatotegegemeka."

SURA YA 2

a Amu 3:28
Amu 12:5

b Kut 3:8

c Kut 23:27
Kum 2:25
Kum 11:25

d Kut 15:15
Yos 5:1

e Kut 14:21
Kut 15:13, 14

f Hes 21:21-24

g Hes 21:33, 34
Kum 3:3
Yos 9:9, 10

h Kum 4:39
2Nya 20:6
Da 4:35

Safu ya 2

a Yos 6:23

b Ebr 11:31

c Hes 30:2

d Yos 6:23

e Yos 2:14

ngamiza baba yangu na mama yangu, ndugu zangu na dada zangu, na watu wetu wote, mtatuokoa tusife."^a

14 Ndipo wanaume hao wakawambia: "Tutakufa badala yenu!* Ikiwa hamtatoa habari kuhusu mambo yaliyotuleta, tutawatendea kwa upendo mshikamanifu na kwa uaminifu Yehova atakapotupatia nchi hii." **15** Basi akawashusha kwa kamba kupitia dirishani, kwa kuwa nyumba yake ilikuwa imejengwa kwenye ukuta wa jiji.^b **16** Naye akawaambia: "Nendeni milimani mkajifiche huko kwa siku tatu ili wale wanaowafuatia wasiwapate. Kisha wakirudi mnaweza kwenda zenu."

17 Wanaume hao wakasema: "Hatutakuwa na hatia kuhusiana na kiapo ulichotupisha^c **18** isipokuwa, tutakapokuja katika nchi hii, utakuwa umefunga kamba hii nyekundu katika dirisha ambamo utatuteremsha. Wakusanye baba yako, mama yako, ndugu zako, na familia yote ya baba yako ndani ya nyumba hii.^d **19** Ikiwa mtu yeyote atataka nje ya nyumba yako, damu yake itakuwa juu ya kichwa chake mwenyewe, nasi hatutakuwa na hatia. Lakini mtu yeyote aliye ndani ya nyumba yako pamoja nawe aki-fa, damu yake itakuwa juu ya vichwa vyetu. **20** Lakini ukitoa habari kuhusu mambo yaliyotuleta,^e hatutakuwa na hatia kuhusiana na kiapo chako ulichotupisha." **21** Naye akasema: "Na iwe kama mliyosema."

2:13 *Au "mtaokoa nafsi zetu." 2:14 *Tnn., "Nafsi zetu zitakufa badala ya nafsi zenu!"

Kwa hiyo akawaruhusu wae-nde zao, nao wakaondoka. Baadaye, akafunga ile kamba nyekundu dirishani. **22** Basi wakaondoka na kuelekea milimani, wakakaa huko kwa siku tatu, mpaka wale waliokuwa wakiwafuatia waliporudi. Waliwatafuta katika kila barabara lakini hawakuwapata. **23** Kisha wapelelezi hao wawili wakaondoka milimani, wakavuka mto na kwenda kwa Yoshua mwana wa Nuni. Wakamsimulia mambo yote yaliyowapata. **24** Halafu wakamwambia hivi Yoshua: “Yehova ametupatia nchi yote.^a Na kwa hakika waakaaji wote wa nchi wamevunjika moyo kwa sababu yetu.”^b

3 Ndipo Yoshua na Waisraeli wote* wakaamka asubuhi na mapema na kusafiri kutoka Shitimu^c mpaka Yordani. Wakalala hapo usiku kabla ya kuvuka.

2 Baada ya siku tatu, viongozi^d walipita kambini **3** na kuwaamuru watu, “Mara tu mtakapoliona sanduku la agano la Yehova Mungu wenu likiwa limebebwa na makuhani Walawi,^e mwondoke na kulifuata, **4** ili mjue njia ya kupita kwa kuwa hamjawahi kupita njia hiyo, lakini muwe umbali wa mikono 2,000* hivi kutoka kwenye sanduku hilo; msilikaribie zaidi.”

5 Kisha Yoshua akawaambia watu: “Jitakaseni,^f kwa maana kesho Yehova atafanya mambo yanayostaajabisha kati yenu.”^g

6 Halafu Yoshua akawaambia makuhani: “Bebeni sa-

3:1 *Tnn., “wana wote wa Israeli.” 3:4 *Karibu mita 890 (futi 2,920). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 2

a Kut 23:31
Yos 6:2
Yos 21:44

b Kut 15:14-16
Yos 2:9-11
Yos 5:1

SURA YA 3

c Hes 25:1
Yos 2:1

d Kum 1:15
Yos 1:10,11

e Hes 4:15
1Nya 15:2

f Kut 19:10
Law 20:7

g Kut 34:10

Safu ya 2

a Kut 25:10
Hes 4:15

b Yos 4:14

c Yos 1:5,17

d Kut 3:12
Kut 14:31

e Yos 3:17

f Kum 7:21

g Kut 3:8
Kum 7:1
Zb 44:2

h Yos 4:2,3

i Zb 114:1,3

j Kut 25:10
Yos 3:6
Mdo 7:44,45

nduku la agano^a na muwata-ngulie watu.” Basi wakabeba sanduku la agano na kuwata-ngulia watu.

7 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: “Leo nitaanza kukukweza machoni pa Waisraeli wote,^b ili wajue kwamba nitakuwa pamoja nawe^c kama nilivyokuwa pamoja na Musa.^d **8** Waamuru hivi makuhani wanaobeba sanduku la agano: ‘Mtakapofika kwenye ukingo wa maji ya Yordani, ingieni na kusimama tuli ndani ya maji ya Yordani.’”^e

9 Yoshua akawaambia Waisraeli: “Njooni hapa msikilize maneno ya Yehova Mungu wenu.” **10** Kisha Yoshua akasema: “Kwa njia hii mtajua kwamba Mungu aliye hai yumo miongoni mwenu,^f na bila shaka atawafukuza mbele yenu Wakanaani, Wahiti, Wahivu, Waperizi, Wagirgashi, Waamori, na Wayebusi.^g **11** Tazameni! Sanduku la agano la Bwana wa dunia nzima linawatangulia kuingia ndani ya Yordani. **12** Sasa chagueni wanau-me 12 kutoka katika makabila ya Israeli, yaani, kila kabila mtu mmoja,^h **13** na mara tu nyayo za makuhani wanaobeba Sanduku la Yehova, Bwana wa dunia nzima, zitakapogusa maji ya Yordani, maji ya Yordani yanayotoka upande wa juu yatasimamishwa, yatakuwa tuli kama bwawa.”ⁱ

14 Basi watu walipotoka ndani ya mahema yao kabla tu ya kuvuka Yordani, makuhani waliobeba sanduku la agano^j wakawatangulia watu. **15** Mara tu makuhani waliobeba lile Sanduku walipofika

3:13 *Au “ukuta.”

Yordani na kutumbukiza miguu yao ukingoni mwa mto huo (kwa maana maji ya Yordani hufurika kwenye kingo zake^a sikuzote za mavuno), **16** maji yanayotoka upande wa juu yakaacha kutiririka. Yakasimama tuli kama bwa-wa* mbali sana huko Adamu, jiji lililo karibu na Sarethani, na yale yanayoshuka kwenye Bahari ya Araba, yaani, Bahari ya Chumvi, yakakauka. Yalisimamishwa, na watu wakavuka kuelekea Yeriko. **17** Makuhani waliobeba sanduku la agano la Yehova wakaendelea kusimama tuli kwenye nchi kavu^b katikati ya Yordani, huku Waisraeli wote wakivuka kwenye nchi kavu^c mpaka taifa lote lilipovuka Yordani.

4 Baada tu ya taifa lote kuvuka Yordani, Yehova akamwambia Yoshua: **2** "Wachukue wanaume 12 kutoka kati ya watu, yaani, mtu mmoja kutoka katika kila kabila,^d **3** na uwaamuru hivi: 'Chukue ni mawe 12 kutoka katikati ya Yordani, mahali ambapo miguu ya makuhani ilisimama tuli,^e myabebe na kuyaweka mahali mtakapolala usiku huu.'"^f

4 Basi Yoshua akawaita wale wanaume 12 aliowachagua kutoka kati ya Waisraeli, yaani, mtu mmoja kutoka katika kila kabila; **5** Yoshua akawaambia: "Nendeni katikati ya Yordani mbele ya sanduku la Yehova Mungu wenu, na kila mmoja wenu abebe jiwe begani, kulingana na idadi ya makabila ya Waisraeli, **6** ili yawe ishara kwenu. Ikiwa watoto* wenu watawauliza wa-

SURA YA 3

a Yos 4:18
1Nya 12:15

b Yos 4:3

c Zb 66:6

SURA YA 4

d Yos 3:12, 13

e Yos 3:17

f Yos 4:19, 20

Safu ya 2

a Kut 13:14
Kum 6:20, 21
Zb 78:3, 4

b Yos 3:13, 16

c Kum 4:9

d Yos 3:17

e Yos 3:8, 17

f Yos 1:12, 14

g Hes 32:20-22
Hes 32:25-29

kati ujao, 'Mawe haya ni ya nini?'"^a **7** waambieni: 'Sanduku la agano la Yehova lilipovushwa Yordani, maji ya Yordani yalizuiwa yasitiririke.^b Basi mawe haya yatakuwa kumbukumbu la kudumu kwa Waisraeli.'"^c

8 Kwa hiyo Waisraeli waka-fanya kama Yoshua alivyowaa-muru. Wakachukua mawe 12 kutoka katikati ya Yordani, kama Yehova alivyomwagiza Yoshua, kulingana na idadi ya makabila ya Waisraeli. Wakayapeleka mahali walipolala usiku na kuyaweka hapo.

9 Pia Yoshua akaweka mawe 12 katikati ya Yordani mahali iliposimama miguu ya makuhani waliobeba sanduku la agano,^d na mawe hayo yako huko mpaka leo.

10 Makuhani waliobeba lile Sanduku waliendelea kusimama katikati ya Yordani mpaka watu walipofanya mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Yoshua, sawasawa na mambo yote ambayo Musa alikuwa amemwamuru Yehova. Wakati huohuo, watu waliharakisha kuvuka. **11** Baada tu ya watu wote kuvuka, makuhani waliobeba Sanduku la Yehova wakavuka huku watu wakiwatazama.^e **12** Na watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase wakavuka wakiwa wamejipanga kivita^f na kuwatangulia Waisraeli wengine, kama Musa alivyokuwa amewaagiza.^g **13** Wanajeshi wapatao 40,000 wakiwa na silaha tayari kwa vita wakavuka mbele za Yehova na kuingia katika jangwa tambarare la Yeriko.

14 Siku hiyo Yehova alimkweza Yoshua machoni pa

Waisraeli wote,^a wakamheshimu sana* sikuzote za maisha yake, kama walivyomheshimu sana Musa.^b

15 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: **16** “Waamuru makuhani wanaobeba sanduku^c la Ushahidi watoke ndani ya Yordani.” **17** Basi Yoshua akawaamuru hivi makuhani: “Tokeni ndani ya Yordani.” **18** Makuhani waliobeba sanduku la agano^d la Yehova walipotoka katikati ya Yordani na nyayo zao kukanyaga nchi kavu, maji ya Yordani yakaanza kutiririka tena na kingo zake zikafurika^e kama mwanzoni.

19 Watu walivuka Yordani siku ya kumi ya mwezi wa kwanza na kupiga kambi Gilgali^f kwenye mpaka wa mashariki wa Yeriko.

20 Kisha Yoshua akapanga kule Gilgali yale mawe 12 ambayo walichukua kutoka Mto Yordani.^g **21** Akawaambia hivi Waisraeli: “Wato-tu wenu watakapowauliza wakati ujao, ‘Mawe haya ni ya nini?’^h **22** Waambieni, ‘Waisraeli walivuka katikati ya Mto Yordani kwenye nchi kavu’ **23** Yehova Mungu wenu alipoyakausha maji ya Yordani mbele yao mpaka walipovuka, kama Yehova Mungu wenu alivyoikausha Bahari Nyekundu* mbele yetu mpaka tulipovuka.^j **24** Alifanya hivyo ili watu wote duniani wajue jinsi mkonu wa Yehova ulivyo na nguvu^k na ili ninyi mmwogope Yehova Mungu wenu sikuzote.”

4:14 *Tnn., “wakamwogopa.” 4:23 *Au “Bahari ya Shamu.”

SURA YA 4

a Yos 3:7

b Kut 14:31

c Kut 25:22

d Hes 4:15

e Yos 3:13, 15

f Yos 4:3
Yos 5:8, 9
Yos 10:6

g Yos 4:8

h Zb 44:1

i Yos 3:17
Zb 66:6j Kut 14:21
Isa 63:12
Ebr 11:29k Kut 9:16
Kut 15:6
Kum 28:10
1Sa 17:46
2Fa 19:19
Zb 106:8

Safu ya 2

SURA YA 5

a Mwa 10:15, 16

b Hes 13:29

c Kut 15:15
Yos 2:24

d Yos 2:9-11

e Mwa 17:9-11

f Yos 5:8, 9

g Hes 14:29
Hes 26:65
Kum 2:14h Hes 14:33
Kum 1:3

i Hes 14:22, 23

j Kum 1:35

k Mwa 13:14, 15
Kut 33:1l Kut 3:8
Hes 13:26, 27
Eze 20:6

m Hes 14:31

5 Mara tu wafalme wote wa Waamori^a waliokuwa upande wa magharibi* wa Yordani na wafalme wote wa Wakanaani^b waliokuwa karibu na bahari waliposikia kwamba Yehova alikausha maji ya Yordani mpaka Waisraeli walipovuka, wakafa moyo^{*c} na hawakuwa na ujasiri wowote kwa sababu ya Waisraeli.^d

2 Wakati huo Yehova akamwambia hivi Yoshua: “Tenge-neza visu vya jiwe gumu na uwatahiri^e wanaume Waisraeli tena, mara ya pili.” **3** Basi Yoshua akatengeza visu vya jiwe gumu na kuwatahiri wanaume Waisraeli kule Gibeath-haaralothi.*^f **4** Yoshua aliwatahiri kwa sababu wanaume wote waliotoka Misri, yaani, wanaume wote wa kwenda vitani,* walikufa nyikani walipotoka Misri.^g **5** Kwa maana watu wote waliotoka Misri walikuwa wametahiriwa, lakini watu wote waliozaliwa nyikani wakiwa safarini kutoka Misri hawakuwa wametahiriwa. **6** Waisraeli walitembea miaka 40^h nyikani mpaka tafia lote lilipokufa, yaani, wanaume wote wa kwenda vitani waliotoka Misri ambao hawakutii sauti ya Yehova.ⁱ Yehova aliwaapia kwamba hatawaruhusu kamwe waione nchi ambayo Yehova alikuwa ame-waapia mababu zao kwamba atatupatia,^k nchi inayotiririka maziwa na asali.^l **7** Kwa hiyo, akawainua wanao badala yao.^m Yoshua akawatahiri

5:1 *Tnn., “upande unaoelekea baharini.” *Tnn., “mioyo yao ikayeyuka.” 5:3 *Maana yake “Kilima cha Magovi.” 5:4 *Au “wanaume wote wenye umri wa kwenda vitani.”

wana hao kwa sababu hawakuwa wametahiriwa safarini.

8 Walipomaliza kutahiri tifa lote, wakaendelea kukaa kambini mpaka walipoona.

9 Kisha Yehova akamwambia Yoshua: "Leo nimewoondolea aibu ya Misri." Basi tangu wakati huo mahali hapo panaitwa Gilgali.*^a

10 Waisraeli wakaendelea kupiga kambi Gilgali, nao wakaadhimisha Pasaka siku ya 14 ya mwezi huo,^b wakati wa jioni, katika jangwa tambarare la Yeriko. **11** Kesho yake, baada ya Pasaka, siku hiyohiyo wakaanza kula mazao ya nchi, yaani, mikate isizo na chachu^c na nafaka zilizokaangwa. **12** Mana ilikoma siku iliyofuata, baada ya Waisraeli kula baadhi ya mazao ya nchi; Waisraeli hawakupata mana tena,^d wakaaanza kula mazao ya nchi ya Kaanaani mwaka huo.^e

13 Yoshua alipokuwa kariibu na Yeriko, aliinua macho na kumwona mwanamume^f fulani amesimama mbele yake akiwa ameshika upanga uliochomolewa.^g Yoshua akamkaribia na kumuuliza: "Uko upande wetu au wa maadui wetu?" **14** Akamjibu: "Hapana, mimi ni mkuu* wa jeshi la Yehova."^h Basi Yehova akaanguka chini kifudifudi, akasujudu, na kumwambia: "Bwana wangu una ujumbe gani kwangu mimi mtumishi wako?" **15** Mkuu wa jeshi la Yehova akamjibu hivi Yoshua: "Vua viatu vyako, kwa sababu mahali unaposisimama ni patakatifu." Yoshua akavua mara moja.ⁱ

5:9 *Maana yake "Kuondoa; Kuondolea Mbali." 5:14 *Au "kiongozi."

SURA YA 5

a Yos 4:19
Yos 5:3

b Kut 12:24, 25
Hes 9:5

c Kut 12:18

d Kut 16:35

e Kum 6:10-12
Kum 8:10

f Mwa 18:2
Amu 13:6
Mdo 1:10

g Kut 23:23
Hes 22:23
1Nya 21:16

h Kut 23:20
1Fa 22:19
Da 10:13

i Kut 3:4, 5

Safu ya 2

SURA YA 6

a Yos 2:9

b Hes 14:9
Kum 7:24
Ne 9:24

c Amu 7:22

d Ebr 11:30

e Hes 4:15

f Hes 10:14,
18, 22
Yos 1:12, 14

6 Basi malango ya jiji la Yeriko yalikuwa yamefungwa kabisa kwa sababu ya Waisraeli; hakuna mtu yeyote aliyetoka wala kuingia.^a

2 Yehova akamwambia Yoshua, "Tazama, nimetia mikononi mwako Yeriko, mfalme wake, na mashujaa wake hodari.^b **3** Ninyi nyote wanaume wa vita mnapaswa kulizunguka jiji hili, lizungukeni mara moja kwa siku. Mtafanya hivyo kwa siku sita. **4** Waagize makuhani saba wabebe pembe saba za kondoo dume na kuli-tangulia Sanduku. Lakini siku ya saba, mnapaswa kulizunguka jiji mara saba na makuhani watapiga pembe hizo.^c **5** Pembe za kondoo dume zitakapopigwa, na mara tu mtakaposikia mlio wake,* watu wote watapiga kelele kubwa za vita. Kisha ukuta wa jiji utaanguka chini,^d na kila mtu ataingia jijini moja kwa moja."

6 Basi Yoshua mwana wa Nuni akawaita makuhani na kuwaambia: "Bebeni sanduku la agano, na makuhani saba wabebe pembe saba za kondoo dume na kulitangulia Sanduku la Yehova."^e **7** Kisha akawaambia watu, "Nendeni mzunguke jiji, na wanajeshi wenye silaha^f walitangulie Sanduku la Yehova."^g **8** Watu wakafanya kama Yoshua alivyowaambia, makuhani saba waliobeba pembe saba za kondoo dume mbele za Yehova, wakatangulia na kupiga pembe hizo, na sanduku la agano la Yehova lilikuwa likiwafuata. **9** Na wanajeshi wenye silaha waliwatangulia makuhani

6:5 *Au "pembe zikipigwa kwa muda mrefu."

waliokuwa wakizipiga pembe, na walinzi wa nyuma walilifuata Sanduku huku pembe ziki-pigwa mfululizo.

10 Yoshua alikuwa ame-waamuru hivi watu: “Msipi-ge kelele wala kupaza sauti. Msiseme neno lolote mpaka siku nitakapowaambia, ‘Paze-ni sauti!’ Ndipo mtakapopaza sauti.” **11** Akaagiza Sanduku la Yehova lipelekwe kuzunguka jiji mara moja, kisha wakarudi kambini na kulala humo usiku.

12 Asubuhi iliyofuata, Yoshua akaamka mapema, na makuhani wakalibeba Sanduku^a la Yehova, **13** makuhani saba waliobeba pembe saba za kondoo dume walilitangulia Sanduku la Yehova wakipiga pembe hizo mfululizo. Nao wanajeshi wenye silaha walitembea mbele yao na walinzi wa nyuma walilifuata Sanduku la Yehova huku pembe zikipigwa mfululizo. **14** Siku ya pili, walilizunguka jiji mara moja, kisha wakarudi kambini. Walifanya hivyo kwa siku sita.^b

15 Siku ya saba wakaamka asubuhi na mapema, wakalizinguka jiji kama kawaida. Ni siku hiyo peke yake ambayo walilizunguka jiji mara saba.^c **16** Na mara ya saba, makuhani walipiga pembe na Yoshua akawaambia watu: “Paze-ni sauti,^d kwa kuwa Yehova amewapa jiji hili! **17** Jiji na vitu vyote vilivyomo vinapaswa kuharibiwa;^e vyote ni vya Yehova. Ila msimwanga-mize Rahabu^f yule kahaba na wote walio pamoja naye nyumbani mwake, kwa sababu aliwaficha wajumbe tuliowatuma.^g **18** Lakini mjepushe na kitu chochote kinachopaswa

SURA YA 6

a 1Nya 15:2

b Yos 6:3

c Yos 6:4

d Yos 6:5, 10

e Law 27:29
Kum 7:2
Kum 20:16f Yos 2:1
Mt 1:5
Ebr 11:31g Mwa 12:3
Yos 2:4, 6
Yak 2:25

Safu ya 2

a Kum 7:26

b Kum 13:17
Yos 7:11, 21

c Yos 7:25

d Hes 31:22, 23

e Yos 6:24
1Fa 7:51
1Nya 18:11

f Yos 6:4, 16

g Yos 6:5
Ebr 11:30h Kum 7:2
Kum 20:16i Yos 2:14
Ebr 11:31j Yos 2:12, 13
Yos 2:17-19

k Yos 6:19

l Yos 2:14
Yos 6:17, 22

kuharibiwa,^a ili msikitamani kitu kinachopaswa kuharibiwa na kukichukua,^b msije mkaleta msiba* kwenye kambini ya Waisraeli.^c **19** Lakini fedha yote na dhahabu na vitu vya shaba na chuma ni vitakatifu kwa Yehova.^d Vinapaswa kupelekwa katika hazina ya Yehova.”^e

20 Basi watu wakapaza sauti pembe zilipopigwa.^f Na mara tu watu waliposikia sauti za pembe na kupiga kelele kubwa za vita, ukuta ukaa-nguka chini.^g Kisha kila mtu akaingia jijini moja kwa moja, nao wakaliteka. **21** Wakaa-ngamiza kwa upanga kila kiumbe kilichokuwa jijini, wanau-me na wanawake, vijana na wazee, ng’ombe dume, kondoo, na punda.^h

22 Yoshua akawaambia wale wanaume wawili walio-kuwa wameipeleleza nchi: “Nendeni katika nyumba ya yule mwanamke kahaba, mkamotoe nje pamoja na watu wake wote, kama mliyomwapa.”ⁱ **23** Basi wale vijana wapelelezi wakaenda kumtoa Rahabu, baba yake, mama yake, ndugu zake, na watu wote wa nyumba yake; naam, wakaitoa nje familia yake yote,^j na kuletela salama salimini nje ya kambini ya Waisraeli.

24 Kisha wakaliteketeza jiji pamoja na kila kitu kilichokuwemo. Lakini fedha, dhahabu, na vitu vya shaba na chuma, wakaviweka katika hazina ya nyumba ya Yehova.^k **25** Yoshua hakumwanga-miza Rahabu yule kahaba, watu wa nyumba ya baba yake, na familia yake yote;^l Rahabu ankaa

6:18 *Au “shida; laana.”

katika Israeli mpaka leo,^a kwa sababu aliwaficha wajumbe waliotumwa na Yoshua kupeleleza Yeriko.^b

26 Wakati huo Yoshua alitangaza kiapo* hiki: “Na alaaniwe mbele za Yehova mtu atakayejaribu kulijenga tena jiji hili la Yeriko. Atakapojenga msingi wake, mzaliwa wake wa kwanza atakufa, na atakapoweke malango yake, mwana wake wa mwisho atakufa.”^c

27 Basi Yehova alikuwa pamoja na Yoshua,^d na umaarufu wake ukaenea duniani pote.^e

7 Lakini Waisraeli walikosa uaminifu kuhusiana na vitu vilivyopaswa kuharibiwa, kwa kuwa Akani^f mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila la Yuda, alichukua baadhi ya vitu vilivyopaswa kuharibiwa.^g Ndipo hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Waisraeli.^h

2 Basi Yoshua akatuma wanaume kutoka Yeriko waende Ai,ⁱ karibu na Beth-aveni, upande wa mashariki wa Betheli,^j akawaambia: “Pandeni mkaipeleleze nchi.” Kwa hiyo wanaume hao wakapanda na kwenda kupeleleza jiji la Ai. **3** Waliporudi kwa Yoshua, wakamwambia: “Si lazima watu wote waende. Wanaume elfu mbili au elfu tatu hivi wanatosha kulishinda jiji la Ai. Usiwachoshe watu wote kwa kuwatuma huko, kwa sababu jiji hilo lina watu wachache tu.”

4 Basi wanaume wapatao 3,000 wakapanda huko, lakini wakakimbizwa na wanaume wa Ai.^k **5** Na wanaume hao wa Ai wakawaua watu 36, wa-

6:26 *Au labda, “aliwaapisha watu kiapo.”

SURA YA 6

a Mt 1:5

b Ebr 6:10
Yak 2:25

c 1Fa 16:34

d Kum 31:6
Yos 1:5e Yos 9:1, 2
Yos 9:9, 10

SURA YA 7

f Yos 22:20
1Nya 2:7

g Kum 7:26

h Yos 6:17, 18

i Mwa 12:8

j Mwa 28:19

k Law 26:14, 17
Kum 28:15, 25
Kum 32:30

Safu ya 2

a Kum 32:26, 27
Zb 106:8
Zb 143:11
Eze 20:9

b Kut 24:7

c Yos 6:17

d Kut 20:15

e Yos 7:21

kawakimbiza kutoka nje ya lango la jiji mpaka Shebarimu,* wakaendelea kuwaua kwenye mteremko. Basi ujasiri wa watu ukayeyuka[#] na kuwa kama maji.

6 Ndipo Yoshua akararua mavazi yake na kuanguka chini kifudifudi mbele ya Sanduku la Yehova mpaka jioni, yeye pamoja na wazee wa Israeli, nao wakaendelea kujirushia mavumbi vichwani. **7** Yoshua akasema: “Ole wangu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, kwa nini umewaleta watu hawa njia yote hii na kuwavusha Yordani ili tu kututia mikononi mwa Waamori watuanguamize? Ni afadhali tungeridhika kubaki ng'ambo ile nyingine ya* Yordani! **8** Nakusihi Ee Yehova, niseme nini baada ya Waisraeli kuwakimbiza maadui wao? **9** Wakanaani na wakaaji wote wa nchi hii watakaposikia habari hii, watatuzingira na kufutilia mbali jina letu kutoka duniani, nawe utafanya nini kwa ajili ya jina lako kuu?”^a

10 Yehova akamwambia Yoshua: “Inuka! Kwa nini umelala chini kifudifudi? **11** Waisraeli wametenda dhambi. Wamevunja agano langu^b nililowaa-muru washike. Wamechukua baadhi ya vitu vilivyopaswa kuharibiwa,^c wameviiba^d na kuvificha kati ya vitu vyao.^e **12** Kwa hiyo, Waisraeli hawa-wezi kusimama dhidi ya maadui wao. Watageuka na kuwakimbiza maadui wao, kwa sababu wanapaswa kuangamizwa. Sitakuwa pamoja nanyi

7:5 *Maana yake “Machimbo.” [#]Tnn., “mioyo ya watu ikayeyuka.” 7:7 *Yaani, upande wa mashariki wa.

tena msipoharibu kitu mlichonacho kinachopaswa kuharibiwa.^a **13** Inuka uwatakase watu!^b Waambie, 'Jitakaseni kwa ajili ya kesho, kwa sababu Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: "Kuna kitu kinachopaswa kuharibiwa miongoni mwenu, Ee Israeli. Hamtaweza kusimama dhidi ya maadui wenu msipoondoa kitu kinachopaswa kuharibiwa. **14** Mtakusanyika asubuhi, kabila kwa kabila, na kabila ambalo Yehova atachagua^c litakaribia, ukoo kwa ukoo, na ukoo ambao Yehova atachagua utakaribia, nyumba kwa nyumba, na nyumba ambayo Yehova atachagua itakaribia, mwanamume kwa mwanamume. **15** Mtu atakayepatikana akiwa na kitu kinachopaswa kuharibiwa atateketewa kwa moto,^d yeye pamoja na vitu vyake vyote, kwa sababu amevunja agano^e la Yehova na kwa sababu ametenda jambo la aibu katika Israeli."'''

16 Kesho yake, Yoshua akaamka asubuhi na mapeema akawakusanya Waisraeli, kabila kwa kabila, na kabila la Yuda likachaguliwa. **17** Kisha akaleta karibu koo za Yuda na ukoo wa Wazera^f ukachaguliwa, kisha akaleta karibu familia za ukoo wa Wazera, mwanamume kwa mwanamume, na Zabdi akachaguliwa. **18** Mwishowe akaleta karibu familia ya Zabdi, mwanamume kwa mwanamume, naye Akani mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila la Yuda, akachaguliwa.^g **19** Kisha Yoshua akamwambia Akani: "Tafadhali mwanangu, mheshimu Yehova Mungu wa Israeli na uungame kwake. Tafadhali

SURA YA 7

a Kum 7:26
Yos 6:18
Isa 59:2

b Kut 19:10

c Met 16:33

d Yos 1:18
Yos 7:25

e Kut 24:7

f Mwa 38:30
Hes 26:20
1Nya 2:4, 6

g Met 16:33
Mdo 5:3

Safu ya 2

a Mwa 10:10

b Yos 22:20

c Yos 6:19

d Yos 15:7, 12
Isa 65:10
Ho 2:15

e Yos 6:18
1Nya 2:7

f Law 24:14
Yos 1:18

g Yos 7:15

niambie jambo ulilofanya. Usinifiche chochote."

20 Akani akamwambia Yoshua: "Kwa kweli ni mimi niliyemtendea dhambi Yehova Mungu wa Israeli, na hili ndilo jambo nililofanya. **21** Nilipoona katika nyara vazi rasmi maridadi kutoka Shinari^a na shekeli 200 za fedha na kipande kimoja cha dhahabu chenye uzito wa shekeli 50,^{*} nilivitamani, kwa hiyo nikavichukua. Nimevificha ardhini ndani ya hema langu, na fedha ziko chini yake."

22 Mara moja Yoshua akutuma wajumbe, wakakimbia kwenda hemani, wakakuta lile vazi likiwa limefichwa ndani ya hema lake, na fedha zilikuwa chini yake. **23** Basi wakavichukua vitu hivyo kutoka hemani na kumletea Yoshua na Waisraeli wote na kuviweka mbele za Yehova. **24** Yoshua na Waisraeli wote wakamchukua Akani^b mwana wa Zera, zile fedha, lile vazi rasmi maridadi, na kile kipande cha dhahabu,^c pamoja na wanawe, binti zake, ng'ombe dume wake, punda wake, kondoo na mbuzi wake, hema lake, na vitu vyake vyote, wakavileta katika Bonde la* Akori.^d **25** Yoshua akasema: "Kwa nini umetuletea msiba?^{*e} Leo Yehova atakuletea msiba." Ndipo Waisraeli wote wakawapiga mawe,^f kisha wakawatekeza kwa moto.^g Naam, waliwapiga mawe wote. **26** Nao wakarundika mawe mengi juu yake ambayo yapo hadi leo. Ndipo hasira ya Ye-

7:21 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.
7:24 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."
7:25 *Au "shida; laana."

hova ikapoa.^a Ndiyo sababu tangu siku hiyo mahali hapo panaitwa Bonde la Akori.*

8 Kisha Yehova akamwambia Yoshua: “Usiogope wala usihofu.^b Nenda na wanajeshi wote ulishambulia jiji la Ai. Naam, nimentia mikononi mwako mfalme wa Ai, watu wake, jiji lake, na nchi yake.^c **2** Mlitendee Ai na mfalme wake kama mlivyolitendee Yeriko na mfalme wake,^d lakini mnaweza kujichukulia nyara zake na mifugo yake. Wekeni watu watakaovizia nyuma ya jiji hilo.”

3 Basi Yoshua na wanajeshi wote wakaenda kulishambulia jiji la Ai. Yoshua akachagua mashujaa hodari 30,000 na kuwatuma wakati wa usiku.

4 Akawaamuru hivi: “Mtavizia nyuma ya jiji. Msiende mbali sana na jiji, na nyote kae ni tayari. **5** Mimi na watu walio pamoja nami tutalikaribia jiji, na watakapotoka ili kutushambulia kama walivyofanya mwanzoni,^e tutawakimbia.

6 Watakapotukimbiza, tutawavuta mbali na jiji lao, kwa kuwa watasema, ‘Wanatukimbia kama walivyofanya mwanzoni.’^f Nasi tutaendelea kuwakimbia. **7** Kisha mtatoka mahali mnapovizia na kuliteka jiji; Yehova Mungu wenu atalitia mikononi mwenu. **8** Na mara tu baada ya kuliteka jiji, mnapaswa kuliteketeza kwa moto.^g Mtafanya kama Yehova alivyoagiza. Hayo ndiyo maagizo mtakayofuata.”

9 Kisha Yoshua akawatuma, nao wakaenda kuvizia; wakapiga kambi kati ya Betheli na Ai, upande wa magharibi wa

SURA YA 7

a Kum 13:17

SURA YA 8

b Kum 7:18

Kum 31:8

Yos 1:9

Isa 12:2

Ro 8:31

c Zb 44:3

d Yos 6:2, 21

e Yos 7:5

f Yos 8:16

g Yos 8:19, 28

Safu ya 2

a Yos 8:1, 3

b Yos 8:2

c Mwa 28:19

d Yos 8:5

e Yos 8:4

f Yos 8:6

Ai, lakini Yoshua alikaa pamoja na watu usiku huo.

10 Yoshua akaamka asubuhi na mapema, akakusanya wanajeshi, kisha yeye na wazee wa Israeli wakawaongoza hadi Ai. **11** Na wanajeshi wote^a waliokuwa pamoja naye wakapanda na kukaribia mbele ya jiji. Wakapiga kambi upande wa kaskazini wa Ai, na bonde lilikuwa kati yao na Ai. **12** Wakati huo, alikuwa ameweka wanajeshi wapatao 5,000 wavizie^b kati ya Betheli^c na Ai, upande wa magharibi wa jiji. **13** Basi kikosi kikubwa kilikuwa upande wa kaskazini wa jiji^d na wanajeshi waliokuwa wakivizia nyuma walikuwa upande wa magharibi wa jiji,^e na usiku huo Yoshua akaenda katikati ya bonde.*

14 Na mara tu mfalme wa Ai alipoona hilo, yeye pamoja na wanaume wa jiji wakaaamka mapema na kwenda haraka kupigana na Waisraeli mahali fulani ng'ambo ya jangwa tambarare. Lakini hakujua kwamba kulikuwa na wanajeshi waliokuwa wakivizia nyuma ya jiji. **15** Watu wa Ai walipowashambulia, Yoshua na wanajeshi wote Waisraeli wakakimbia barabarani kuelekea nyikani.^f **16** Ndipo watu wote waliokuwa ndani ya jiji wakaambiwa wawakimbize; na walipokuwa wakimkimbiza Yoshua, walienda mbali na jiji. **17** Hakuna mwanamume yeyote aliyebaki Ai na Betheli, wote waliwakimbiza Waisraeli. Waliacha jiji lao wazi na kuwakimbiza Waisraeli.

18 Sasa Yehova akamwambia Yoshua, “Nyoosha mkuki

7:26 *Maana yake “Msiba; Laana.”

8:13 *Au “nchi tambarare ya chini.”

ulio mkononi mwako kuelekea Ai,^a kwa maana nitalitia jiji hilo mikononi mwako.”^b Basi Yoshua akanyoosha mkuiki uliokuwa mkononi mwake kuelekea jiji hilo. **19** Na mara tu aliponyoosha mkono wake, wanajeshi waliokuwa wakivizia wakatoka haraka mahali walipokuwa, wakakimbia kuingia jijini, na kuliteka jiji hilo. Na mara moja wakaliteketeza.^c

20 Wanaume wa Ai walipogeuka na kuangalia nyuma, wakaona moshi ukipanda angani kutoka jijini, wakaishwa na nguvu na hawakuweza kukimbia upande wowote. Kisha wanajeshi Waisraeli waliokuwa wakikimbia kuelekea nyikani wakageuka na kuanza kuwashambulia wale waliokuwa wakiwakimbiza. **21** Yoshua na Waisraeli wote walipoona kwamba wanajeshi waliovizia walikuwa wameliteka jiji na kuona moshi ukipanda kutoka jijini, wakageuka na kuwashambulia wanaume wa Ai. **22** Na wale walioiteka jiji wakaenda kuungana na wenzao, na wanaume wa Ai wakanaswa katikati, baadhi ya Waisraeli walikuwa upande huu na wengine upande wa pili, wakawaua na hakuna yeyote aliyeokoka wala kuponyoka.^d **23** Lakini walimkamata mfalme wa Ai^e akiwa hai na kumpeleka kwa Yoshua.

24 Baada ya Waisraeli kumaliza kuwaua wakaaji wote wa Ai nyikani, ambako waliwafuatia na kumuua kila mmoja wao kwa upanga, Waisraeli wote walirudi Ai na kuwaua kwa upanga watu waliobaki jijini. **25** Watu wote walioangamia siku hiyo, wanaume na wanawake, walikuwa

SURA YA 8

a Kut 17:11
Yos 8:26

b Kum 7:24

c Yos 8:8, 28

d Law 27:29
Kum 7:2

e Yos 8:29
Yos 12:7,9

Safu ya 2

a Kut 17:11
Yos 8:18

b Law 27:29

c Yos 8:2

d Yos 8:8

e Kum 21:22, 23

f Kum 11:29
Kum 27:4, 5

g Kum 31:9
Yos 1:8

h Kut 20:25

i Kum 27:6, 7

j Kum 27:2, 3

k Kut 24:4
Kut 34:27

l Law 24:22
Hes 15:16

12,000, yaani, watu wote wa Ai. **26** Yoshua hakuushusha mkono wake uliokuwa ume-shika mkuki^a mpaka alipowaangamiza wakaaji wote wa Ai.^b **27** Hata hivyo, Waisraeli walijichukulia mifugo na nyara za jiji kama Yehova alivyo-mwagiza Yoshua.^c

28 Kisha Yoshua akateketeza jiji la Ai, na tangu siku hiyo likabaki rundo la kudumu la magofu.^d **29** Akamtundika mtini mfalme wa Ai mpaka jioni, na jua lilipokaribia kutua, Yoshua akaagiza maiti yake iondolewe mtini.^e Kisha wakaaitupa kwenye lango la jiji na kurundika mawe mengi juu ya maiti hiyo, na rundo hilo lipo mpaka leo.

30 Kisha Yoshua akamjengea Yehova Mungu wa Israeli madhabahu kwenye Mlima Ebali,^f **31** kama Musa mtumishi wa Yehova alivyowaa-muru Waisraeli na kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Sheria^g ya Musa: “Madhabahu ya mawe ambayo hayakucho-ngwa wala kuguswa na kifaa chochote cha chuma.”^h Na juu yake wakamtolea Yehova dhabihu za kuteketezwa na pia dhabihu za ushirika.ⁱ

32 Kisha akiwa huko akaandika juu ya mawe hayo nakala ya Sheria^j ambayo Musa alikuwa ameandika mbele ya Waisraeli.^k **33** Waisraeli wote pamoja na wazee wao, viongozi wao, na waamuzi wao, walikuwa wamesimama pande mbili za hilo sanduku la agano la Yehova mbele ya makuhani Walawi waliokuwa wamelibeba. Wakaaji wage-ni na pia wenyeji walikuwepo.^l Nusu yao walisimama mbele ya Mlima Gerizimu, na nusu

walisimama mbele ya Mlima Ebali^a (kama Musa mtumishi wa Yehova alivyokuwa amea-giza mwanzoni),^b ili kuwabariki Waisraeli. **34** Kisha Yoshua akasoma kwa sauti maneno yote ya Sheria,^c baraka^d na laana,^e kulingana na yote ambayo yameandikwa katika kitabu cha Sheria. **35** Haku-na neno lolote kati ya mane-no yote ambayo Musa aliku-wa ameamuru ambalo Yoshua hakusoma kwa sauti mbele ya kutaniko lote la Israeli,^f lililolitia ndani wanawake, watoto, na wakaaji wageni^g walioishi* miongoni mwao.^h

9 Waliposikia habari hizo, wafalme wote waliokuwa upande wa magharibi wa Yordani,ⁱ katika eneo lenye milima, na Shefela, na eneo lote la pwani ya Bahari Kuu,^j na mbele ya Lebanoni—Wahiti, Waamori, Wakanaanani, Wape-rizi, Wahivi, na Wayebusi^k—**2** wakaungana ili kupigana na Yoshua na Waisraeli.^l

3 Wakaaji wa Gibeoni^m walisikia pia mambo ambayo Yoshua alitenda katika jiji la Yerikoⁿ na Ai.^o **4** Basi wakatenda kwa busara na kuweka vyakula katika magunia yaliyochakaa na kuyabeba kwa punda wao, pamoja na viriba vya divai vilivyochakaa na kutiwa viraka; **5** pia walivaa viatu vilivyochakaa vyenye viraka na nguo zilizochakaa. Na mikate waliyobeba ilikuwa imekauka na kuvunjika-vunjika. **6** Kisha wakaenda kwa Yoshua kam-bini kule Gilgali,^p wakamwambia yeye na wazee wa Waisraeli: “Tumetoka nchi ya mba-

8:35 *Tnn., “waliotembea.” **9:1** *Yaani, Mediterania.

SURA YA 8

a Kum 27:12, 13

b Kum 11:29

c Kum 31:9
Ne 8:3

d Kum 28:2

e Kum 27:15
Kum 28:15f Kum 4:2
Kum 12:32g Law 24:22
Hes 15:16h Kum 29:10, 11
Kum 31:12
Ne 8:2

SURA YA 9

i Yos 12:7, 8

j Hes 34:2, 6

k Mwa 15:18-21
Kut 3:17
Kut 23:23
Kum 7:1

l Yos 24:11

m Yos 10:2
Yos 11:19

n Yos 6:20

o Yos 8:24

p Yos 5:10
Yos 10:43

Safu ya 2

a Mwa 10:15, 17
Mwa 34:2
Kut 3:8b Kut 34:12
Kum 7:2
Kum 20:16-18

c Kum 20:10, 15

d Kut 9:16
Kut 15:13, 14
Yos 2:9, 10e Hes 21:21-24
Kum 2:32-34f Hes 21:33-35
Kum 3:3

g Kum 20:10, 11

h Yos 9:6

i Yos 9:5

j Yos 9:4

k Hes 27:18, 21
1Sa 30:7, 8

l Yos 11:19

li. Basi fanyeni agano pamoja nasi.” **7** Lakini wazee wa Waisraeli wakawaambia hao Wahivi:^a “Huenda mnakaa karibu nasi. Tunawezaje kufanya agano nanyi?”^b **8** Wakamjibu Yoshua: “Sisi ni watumishi* wako.”

Kisha Yoshua akawauliza: “Ninyi ni nani, na mnatoka wapi?” **9** Wakamjibu: “Sisi watumishi wako tumetoka nchi ya mbali sana^c kwa sababu ya heshima ya jina la Yehova Mungu wako, kwa kuwa tumesikia umaarufu wake na mambo yote aliyotenda Misri^d **10** na mambo yote aliyowatendea wale wafalme wawili wa Waamori waliokuwa ng’ambo ya* Yordani, yaani, Mfalme Sihoni^e wa Heshboni na Mfalme Ogu^f wa Bashani, aliyekuwa Ashtarothi. **11** Kwa hiyo wazee wetu na wakaaji wote wa nchi yetu wakatuambia, ‘Bebeni chakula kwa ajili ya safari mwende mkakutane nao. Waambieni hivi: “Tutakuwa watumishi wenu;^g basi fanyeni agano pamoja nasi.”’^h **12** Mikate hii ilikuwa moto tulipotoka nyumbani ili kuja hapa. Sasa angalieni jinsi ilivyokauka na inavyovunjika-vunjika.ⁱ **13** Na viriba hivi vilikuwa vipya tulipovijaza divai, lakini sasa vimepasuka.^j Na nguo na viatu vyetu vimechakaa kwa sababu ya safari ndefu.”

14 Ndipo wazee wa Waisraeli wakachukua* vyakula vyao, lakini hawakutafuta mwongozo wa Yehova.^k **15** Basi Yoshua akafanya amani nao,^l pia akafanya agano pamoja nao ili kuwaacha waishi, na hivyo

9:8 *Au “watumwa.” **9:10** *Yaani, upande wa mashariki wa. **9:14** *Au “wakakagua.”

ndivyo wakuu wa Waisraeli walivyowaapia.^a

16 Siku tatu baada ya kufanya agano pamoja nao, wakashika kwamba walikuwa majirani wao na waliishi kariibu nao. **17** Ndipo Waisraeli wakaanza safari na kufika katika majiji ya watu hao siku ya tatu; na majiji yao yalikuwa Gibeoni,^b Kefira, Beerothi, na Kiriath-yearimu.^c **18** Lakini Waisraeli hawakuwashambulia, kwa sababu wakuu wa Waisraeli walikuwa wamewaapia kwa jina la Yehova^d Mungu wa Israeli. Kwa hiyo Waisraeli wote wakaanza kuwanung'unikia wakuu hao. **19** Basi wakuu wote wakaambia hivi: "Kwa kuwa tuliwaapia kwa jina la Yehova Mungu wa Israeli haturuhusiwi kuwadhuru. **20** Hili ndilo jambo tutakalofanya: Tutawaacha waishi, ili hasira ya Mungu isiwake dhidi yetu kwa sababu ya kiapo tulichowaapia."^e **21** Wakuu wakaendelea kuwaambia hivi: "Wacheneni waishi, lakini watakuwa wakusanyaji wa kuni na watekaji wa maji kwa ajili ya Waisraeli wote." Hivyo ndivyo wakuu walivyowaahidi.

22 Basi Yoshua akawaita na kuwauliza: "Kwa nini mlitudanganya mkisema, 'Tumetoka mbali sana,' na kumbe mnaishi karibu kabisa nasi?"^f **23** Kuanzia sasa mmelaaniwa,^g na sikuzote mtakuwa watumwa wa kukusanya kuni na kuteka maji kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu." **24** Ndipo wakamjibu Yoshua: "Tulifanya hivyo kwa sababu sisi watumishi wako tuliambiwa waziwazi kwamba Yehova Mungu wako alimwamuru Musa mtu-

SURA YA 9

a 2Sa 21:2

b Yos 10:2

c Yos 18:11, 14
1Sa 7:1
1Nya 13:5d Hes 30:2
Kum 6:13e 2Sa 21:1
Zb 15:4
Mhu 5:4, 6

f Yos 9:6, 16

g Mwa 9:25, 26

Safu ya 2

a Kum 7:1
Kum 20:16b Kum 2:25
Kum 11:25
Yos 5:1
Ebr 11:31

c Yos 9:21

d 1Fa 8:29
1Nya 9:2
2Nya 6:6
Ezr 7:24
Ezr 8:17
Ne 3:26
Ne 7:60

SURA YA 10

e Yos 8:24, 29

f Yos 6:2, 21

g Yos 9:9, 15
Yos 11:19h Kum 2:25
Kum 11:25
Yos 2:10, 11
Yos 5:1

i Yos 8:25

j Mwa 23:2
Hes 13:22

k Yos 12:7, 10-12

l Yos 9:9, 15
Yos 11:19

m Mwa 15:16

mishi wake awape ninyi nchi yote na kuwaangamiza wakaaaji wote kutoka mbele yenu.^a Basi tulifanya hivyo kwa sababu tuliogopa mtatua.^b **25** Sasa tuonyeshe rehema.* Tutendee upendavyo." **26** Na hivyo ndivyo alivyofanya; aliwaokoa kutoka mikononi mwa Waisraeli, nao hawakuwaua. **27** Lakini tangu siku hiyo, Yoshua akawafanya kuwa wakuwanyaji wa kuni na watekaji wa maji kwa ajili ya kusanyiko^c na kwa ajili ya madhabahu ya Yehova mahali ambapo Mungu angechagua.^d

10 Mara tu Mfalme Adonisedeki wa Yerusalemu aliposikia kwamba Yoshua ameteka Ai na kuliangamiza, na kulitendea Ai na mfalme wake^e kama alivyolitendea Yeriko na mfalme wake,^f na jinsi wakaaji wa Gibeoni walivyofanya amani na Waisraeli^g na kuendelea kukaa kati yao, **2** akaogopa sana,^h kwa sababu Gibeoni lilikuwa jiji kubwa kama majiji yaliyotawaliwa na mfalme. Lilikuwa kubwa kulioko Ai,ⁱ na wanaume wake wote walikuwa mashujaa. **3** Basi Adonisedeki mfalme wa Yerusalemu akatuma ujumbe huu kwa Hohamu mfalme wa Hebroni,^j Piramu mfalme wa Yarmuthi, Yafia mfalme wa Lakishi, na kwa Debiri mfalme wa Egloni.^k **4** "Njoooni mnisaidie kuwashambulia wakaaji wa Gibeoni, kwa sababu wamefanya amani na Yoshua na Waisraeli."^l **5** Ndipo wafalme wano wa Waamori,^m yaani, mfalme wa Yerusalemu, mfalme wa Hebroni, mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi, na mfal-

9:25 *Tnn., "tumo mikononi mwako."

me wa Egloni wakakusanyika pamoja na majeshi yao, wakae-nda kupiga kambi ili kulishambulia jiji la Gibeoni.

6 Kisha wazee wa Gibeoni wakatuma ujumbe kwa Yoshua kambini Gilgali,^a wakisema: “Usituache* sisi watumwa wako.^b Njoo haraka ili utuo-koie na kutusaidia! Wafalme wote wa Waamori kutoka katika eneo lenye milima wamekusanyika ili kutushambulia.”

7 Basi Yoshua akapanda kutoka Gilgali pamoja na jeshi lake lote na mashujaa hodari.^c

8 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: “Usiwaogope,^d kwa maana nimewatia mikononi mwako.^e Hakuna mtu yeyote kati yao atakayekushinda.”^f

9 Yoshua akawashambulia ghafla baada ya kutembea usiku kucha kutoka Gilgali. **10** Yehova akawavuruga,^g na Waisraeli wakawaangamiza wengi wao kule Gibeoni, wakawafuatia kwenye njia inayopanda kwenda Beth-horoni na kuwaua mpaka Azeka na Makeda. **11** Walipokuwa wakiwakimbia Waisraeli, Yehova akawanyeshea mvua ya mawe makubwa kutoka angani kwenye mteremko wa Beth-horoni mpaka Azeka, nao wakafa. Kwa kweli, wale waliouawa na mvua ya mawe walikuwa wengi kuliko wale waliouawa na Waisraeli kwa upanga.

12 Ni siku hiyo, siku ambayo Yehova aliwashinda kabisa Waamori mbele ya Waisraeli, ndipo Yoshua alipomwambia hivi Yehova mbele ya Waisraeli:

10:6 *Tnn., “Usiulegeze mkono wako kutuelekea.”

SURA YA 10

a Yos 5:10

b Yos 9:25, 27

c Yos 8:3

d Kum 3:2
Kum 20:1

e Kum 7:24
Yos 11:6

f Yos 1:3-5

g Zb 44:3

Safu ya 2

a 2Fa 20:10
Zb 135:6
Isa 38:8

b Isa 28:21

c 2Sa 1:17, 18

d Kum 9:18, 19
1Fa 17:22
Yak 5:16

e Kum 1:30
Yos 23:3

f Yos 5:10
Yos 9:6

g Yos 10:10

h Yos 10:28

i Kum 28:7

“Jua, simama tuli^a juu ya Gibeoni,^b

Na mwezi, juu ya Bonde la* Aiyaloni.”

13 Basi jua likasimama tuli na mwezi ukatulua mpaka tafa la Israeli lilipolipiza kisasi dhidi ya maadui wake. Je, haijaandikwa hivi katika kitabu cha Yashari:^c Jua lilisimama tuli katikati ya mbingu na halikutua kwa siku nzima?

14 Haijawahi kamwe kutokea siku kama hiyo, kabla au baada yake, ambayo Yehova alii-sikiliza sauti ya mwanadamu^d katika njia hiyo, kwa sababu Yehova alikuwa akiwapigania Waisraeli.^e

15 Baada ya mambo hayo Yoshua na Waisraeli wote wakarudi kambini Gilgali.^f

16 Wakati huo, wale wafalme watano walikimbia na kujificha pangoni kule Makeda.^g **17** Yoshua akaambiwa: “Wale wafalme watano wamejificha pangoni kule Makeda.”^h **18** Basi Yoshua akasema: “Bingirisheni mawe makubwa kwenye mwingilio wa pango hilo na kuweka walinzi hapo. **19** Lakini ninyi wengine msikae hapo. Wakimbizeni maadui wenu na kuwashambulia kutokea nyuma.ⁱ Msiwape nafasi ya kuingia katika majiji yao, kwa kuwa Yehova Mungu wenu amewatia mikononi mwenu.”

20 Baada ya Yoshua na Waisraeli kuwaangamiza karibu watu wote na wachache waliobaki kukimbilia katika majiji yenye ngome, **21** Waisraeli wote wakarudi salama kambini kwa Yoshua kule Makeda. Hakuna mtu aliyethubutu

10:12 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”

kusema neno lolote* dhidi ya Waisraeli. **22** Kisha Yoshua akasema, “Fungueni mwingilio wa pango, watoeni nje wale wafalme watano na kuwaleta kwangu.” **23** Basi wakawatoa pangoni wafalme hawa watano na kuwaleta kwake: mfalme wa Yerusalemu, mfalme wa Hebroni, mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi, na mfalme wa Egloni.^a **24** Walipomletea Yoshua wafalme hao, akawaita wanaume wote wa Israeli na kuwaambia makamanda wa jeshi walioenda naye: “Njooni. Wakanyageni nyuma ya shingo wafalme hawa.” Basi wakaja na kuwakanyaga nyuma ya shingo.^b **25** Ndipo Yoshua akawaambia: “Msio gope wala msihofu.^c Iweni jasiri na imara, kwa maana hivi ndivyo Yehova atakavyowatendea maadui wenu wote ambao mnapihana nao.”^d

26 Kisha Yoshua akawapiga na kuwaua, akawatundika juu ya miti mitano, wakaning’inia juu ya miti hiyo mpaka jioni. **27** Na jua lilipotua, Yoshua akaagiza washushwe kutoka kwenye miti^e hiyo na kutupwa ndani ya pango ambamo walikuwa wamejificha. Kisha mawe makubwa yakawekwa kwenye mwingilio wa pango hilo, nayo yapo mpaka leo.

28 Yoshua akateka jiji la Makeda^f siku hiyo na kuwaangamiza wakaaji wake kwa upanga. Akamwangamiza mfalme wake na wakaaji wote, na hakuna mtu yeyote aliyebaki.^g ^g Alimtendea mfalme wa Makeda^h kama alivyomtendea mfalme wa Yeriko.

10:21 * Tnn., “kunoa ulimi wake.” 10:28 * Au “nafsi yoyote iliyobaki.”

SURA YA 10

a Yos 10:3-5
Yos 12:7,10-12

b Kut 23:27

c Kum 31:6
Yos 1:9

d Kum 3:21
Kum 7:18, 19

e Kum 21:22, 23
Yos 8:29

f Yos 10:10
Yos 15:20, 41

g Kum 20:16

h Yos 12:7,16

Safu ya 2

a Yos 15:20, 42
Yos 21:13

b Yos 12:7,15

c Yos 6:2, 21

d Yos 10:3, 4
Yos 12:7, 11
Yos 15:20, 39

e Kum 20:16

f Yos 12:7,12
Yos 16:10
Yos 21:20, 21
1Fa 9:16

g Yos 10:3, 4
Yos 12:7,12
Yos 15:20, 39

h Kum 20:16
Yos 10:32

i Mwa 13:18
Mwa 23:19
Hes 13:22

Yos 10:3, 4
Yos 15:13
Yos 21:13

29 Kisha Yoshua na Waisraeli wote wakatoka Makeda na kwenda Libna, wakalishambulia jiji la Libna.^a **30** Yehova akalitia pia jiji hilo na mfalme wake^b mikononi mwa Waisraeli, wakalishambulia na kuwaangamiza wakaaji wote kwa upanga, na hakuna yeyote aliyebaki humo. Wakamtendea mfalme wake kama walivyomtendea mfalme wa Yeriko.^c

31 Kisha Yoshua na Waisraeli wote wakatoka Libna na kwenda Lakishi,^d wakapiga kambi huko na kulishambulia. **32** Yehova akalitia jiji la Lakishi mikononi mwa Waisraeli, nao wakaliteka siku ya pili. Wakalishambulia na kuwaangamiza wakaaji wote* kwa upanga,^e kama walivyofanya kule Libna.

33 Ndipo Horamu mfalme wa Gezeri^f akaenda kulisaidia Lakishi, lakini Yoshua akamua yeye na watu wake wote, na hakuna yeyote aliyebaki.

34 Kutoka Lakishi, Yoshua na Waisraeli wote wakaenda Egloni,^g wakapiga kambi huko na kulishambulia. **35** Wakaliteka siku hiyo na kuliangamiza kwa upanga. Wakawaangamiza wakaaji wote siku hiyo, kama walivyofanya kule Lakishi.^h

36 Kutoka Egloni, Yoshua na Waisraeli wote wakaenda Hebroniⁱ na kulishambulia. **37** Wakaliteka na kuliangamiza kwa upanga jiji hilo, mfalme wake, miji yake, na wakaaji wote, na hakuna yeyote aliyebaki. Yoshua aliliangamiza pamoja na wakaaji wote,* kama alivyofanya kule Egloni.

10:32 * Tnn., “nafsi zote.” 10:37 * Au “kila nafsi.”

38 Mwishowe Yoshua na Waisraeli wote wakaelekea Debiri^a na kulishambulia.

39 Akaliteka pamoja na mfalme wake, na miji yake yote, wakawaangamiza wakaaji wote kwa upanga,^b na hakuna yeyote aliyebaki.^c Alilite-ndea Debiri na mfalme wake kama alivyolitendea Hebroni na pia Libna na mfalme wake.

40 Hivyo Yoshua akaiteka nchi yote kutia ndani eneo lenye milima, Negebu, Shefela,^d na miteremko, na kuwashinda wafalme wao wote, na hakuna yeyote aliyebaki; alimwangamiza kila kiumbe anayepumua,^e kama Yehova Mungu wa Israeli alivyoamuru.^f **41** Yoshua aliwashinda kuanzia Kadesh-barnea^g mpaka Gaza^h na nchi yote ya Gosheniⁱ kufika Gibeoni.^j **42** Yoshua aliwateka wafalme hao wote na nchi zao kwa wakati mmoja, kwa sababu Yehova Mungu wa Israeli alikuwa akiwapigania Waisraeli.^k **43** Hatimaye Yoshua na Waisraeli wote wakarudi kambiini Gilgali.^l

11 Mara tu Yabini mfalme wa Hasori aliposikia habari hizo, akatuma ujumbe kwa Yobabu mfalme wa Madoni,^m na kwa mfalme wa Shimroni, na mfalme wa Akshafi,ⁿ **2** wafalme wa eneo la kaskazini lenye milima, wa maeneo tambarare* upande wa kusini wa Kinerethi, wale walio-kuwa Shefela na kwenye miteremko ya Dori^o upande wa magharibi, **3** Wakanaani^p upande wa mashariki na magharibi, Waamori,^q Wahiti, Waperizi, Wayebusi katika eneo lenye milima, na Wahivi^r chi-

11:2 *Au "Araba."

SURA YA 10

a Yos 12:7,13
Yos 15:15

b Kum 7:2

c Yos 11:14

d Yos 9:1, 2
Amu 1:9

e Law 27:29
Kum 20:16
Yos 11:14

f Kum 7:2
Kum 9:5

g Hes 34:2, 4
Kum 9:23

h Kum 2:23

i Yos 15:20, 51

j Yos 11:16, 19

k Kut 14:14
Kum 1:30

l Yos 4:19

SURA YA 11

m Yos 12:7, 19

n Yos 12:7, 20

o Yos 17:11
Amu 1:27

p Hes 13:29

q Mwa 15:16

r Kum 7:1
Kum 20:17

Safu ya 2

a Kum 4:48

b Yos 10:8

c Kum 17:16
Met 21:31

d Yos 21:44

e Mwa 10:19
Yos 19:28, 31

f Yos 13:1, 6

g Kum 20:16

h Yos 11:6

i Yos 12:7, 19

j Law 27:29

k Kum 20:16
Yos 11:14

l Kum 9:5

ni ya Mlima Hermoni^a katika nchi ya Mispa. **4** Basi wakatoka na majeshi yao yote, watu wengi sana kama chembe za mchanga kwenye ufuo wa bahari, pamoja na farasi na magari mengi sana ya vita.

5 Wafalme hao wote wakakubaliana kukutana, nao wakaja na kupiga kambi karibu na chemchemi ya Meromu ili kupigana na Waisraeli.

6 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: "Usiwaogope^b kwa sababu kesho, wakati kama huu, nitawatia wote mikononi mwa Waisraeli, nanyi mtawaangamiza. Mtakata mishipa ya miguu ya farasi wao,^c na kuyachoma moto magari yao." **7** Basi Yoshua na wanajeshi wake wote wakawashambulia ghafla karibu na chemchemi ya Meromu. **8** Yehova akawatia mikononi mwa Waisraeli,^d nao wakawashinda na kuwakimbiza mpaka Sidoni Kuu^e na Misrefoth-maimu^f na Bonde la Misper upande wa mashariki, nao wakawaangamiza, na hakuna yeyote aliyebaki.^g

9 Kisha Yoshua akawatendea kama Yehova alivyokuwa amemwambia; akakata mishipa ya miguu ya farasi wao na kuchoma moto magari yao.^h

10 Yoshua akarudi na kuliteka Hasori, akamuua mfalme wake kwa upanga,ⁱ kwa sababu Hasori lilikuwa jiji kuu kati ya falme hizo zote.

11 Wakawaangamiza wakaaji wote* kwa upanga.^j Hakuna kiumbe yeyote anayepumua aliyebaki.^k Kisha akaliteketeza Hasori. **12** Yoshua akayateka majiji yote ya wafalme hao na kuwashinda wafalme wote kwa upanga.^l

11:11 *Au "Wakaziangamiza nafsi zote."

Akawaangamiza,^a kama Musa mtumishi wa Yehova alivyomuru. **13** Hata hivyo, Waisraeli hawakutekeza jiji lolote lililokuwa vilimani isipokuwa Hasori ambalo liliteketewa na Yoshua. **14** Waisraeli wakajichukulia nyara zote na mifugo katika majiji hayo.^b Lakini wakawaangamiza wanadamu wote kwa upanga.^c Hawakumwacha mtu yeyote anayepumua.^d **15** Kama Yehova alivyomwamuru Musa mtumishi wake, ndivyo Musa alivyomwamuru Yoshua,^e na ndivyo Yoshua alivyofanya. Hakuna jambo lolote ambalo hakufanya kati ya mambo yote ambayo Yehova alimwamuru Musa.^f

16 Yoshua aliitaka nchi hii yote: eneo lenye milima, eneo lote la Negebu,^g nchi yote ya Gosheni, Shefela,^h Araba,ⁱ na eneo lenye milima la Israeli na maeneo yake ya Shefela,^{*} **17** kuanzia Mlima Hala-ki, unaopanda hadi Seiri, na hadi Baal-gadi^j katika Bonde la Lebanoni chini ya Mlima Hermoni,^k naye akawashinda, akawakamata, na kuwaua wafalme wote wa maeneo hayo. **18** Yoshua alipigana na wafalme hao wote kwa muda mrefu. **19** Hakuna jiji lolote lililofanya amani na Waisraeli isipokuwa Wahivi waliokaa Gibeoni.^l Waisraeli walipigana na majiji mengine yote na kuyashinda.^m **20** Yehova aliacha mioyo yao iwe mikaidiⁿ hivi kwamba wakapigana na Waisraeli, ili awaangamize bila huruma.^o Walipaswa kuangamizwa, kama Yehova alivyomwamuru Musa.^p

11:16 *Au "maeneo yake yaliyo chini ya milima."

SURA YA 11

- a Kum 7:2, 16
b Yos 8:2, 27
c Kum 7:2
d Kum 20:16
e Kum 3:28
Kum 7:1
Kum 31:7
f Kum 4:2, 5
g Hes 13:17
Kum 1:7
h Yos 10:40, 41
i Yos 12:7, 8
j Yos 13:1, 5
k Kum 4:48
Yos 13:8, 11
l Yos 9:7, 15
m Kum 20:17
n Kum 2:30
o Kut 34:12
Kum 7:2
p Kum 20:16

Safu ya 2

- a Hes 13:22
Kum 1:28
Yos 15:13, 14
b Law 27:29
Yos 11:12
Yos 24:11
c Kut 23:28-30
d Amu 1:18
e 1Sa 17:4
f 2Nya 26:1, 6
g Kut 23:27
Kum 11:23
h Hes 26:53, 54
Yos 14:1
i Yos 14:15
Yos 21:44
Yos 23:1

SURA YA 12

- j Kum 2:24
k Kum 3:8
l Kum 4:47-49
m Hes 21:23, 24
n Kum 3:12
o Hes 21:13
p Yoh 6:1
q Kum 3:27
r Hes 21:33-35
s Kum 3:11

21 Wakati huo, Yoshua aliwaangamiza kabisa Waanaki^a kutoka katika eneo lenye milima, Hebroni, Debiri, Anabu, na kutoka katika eneo lote lenye milima la Yuda na Israeli. Yoshua aliwaangamiza watu hao na majiji yao.^b **22** Waanaki hawakubaki katika nchi ya Waisraeli; walibaki^c tu Gaza,^d Gathi,^e na Ashdodi.^f **23** Basi Yoshua akachukua nchi yote, kama Yehova alivyomwahidi Musa,^g Yoshua akawapa Waisraeli iwe urithi wao ili igawanywe kulingana na makabila yao.^h Nchi ikawa na amani bila vita.ⁱ

12 Basi hawa ndio wafalme ambao Waisraeli waliwashinda na kumiliki nchi yao upande wa mashariki wa Yordani, kuanzia Bonde* la Arnoni^j hadi Mlima Hermoni^k na eneo lote la Araba kuelekea upande wa mashariki:^l **2** Mfalme Sihoni^m wa Waamori, aliyeishi Heshboni na kutawala kutoka Aroeri,ⁿ kwenye ukingo wa Bonde* la Arnoni,^o na kutoka katikati ya bonde hilo, na nusu ya Gileadi hadi Bonde la Yaboki, kwenye mpaka wa Waamoni. **3** Alikawala pia Araba hadi Bahari ya Kinerethi*^p kuelekea mashariki hadi Bahari ya Araba, yaani, Bahari ya Chumvi, upande wa mashariki kuelekea Beth-yeshimothi, na kuelekea kusini chini ya mitermko ya Pisga.^q

4 Pia, eneo la Mfalme Ogur wa Bashani, aliyekuwa kati ya Warefaimu^s waliosalia, ambaye aliishi Ashtarothi na Edrei **5** na kutawala katika eneo la

12:1, 2 *Au "Korongo." **12:3** *Yaani, Ziwa Genesareti, au Bahari ya Galilaya.

Mlima Hermoni, Saleka, na Bashani yote,^a hadi mpaka wa Wageshuri na Wamaakathi,^b na nusu ya Gileadi, hadi kati-ka eneo la Mfalme Sihoni wa Heshboni.^c

6 Musa mtumishi wa Yehova pamoja na Waisraeli waliwashinda,^d kisha Musa mtumishi wa Yehova akawapa nchi hiyo watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase ili waimiliki.^e

7 Hawa ndio wafalme ambao Yoshua na Waisraeli waliwashinda upande wa magharibi wa Yordani, kuanzia Baalgadi^f katika Bonde la Lebanoni^g hadi Mlima Halaki,^h unaopanda hadi Seiri,ⁱ halafu Yoshua akayapa makabila ya Israeli nchi yao ili waimiliki na kugawana kulingana na makabila yao,^j **8** katika eneo lenye milima, Shefela, Araba, kwenye miteremko, nyikani, na katika Negebu^k—nchi ya Wahiti, Waamori,^l Wakanaani, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi:^m

9 Mfalme wa Yeriko,ⁿ mfalme wa Ai,^o jiji lililokuwa kando ya Betheli,

10 mfalme wa Yerusalemu, mfalme wa Heroni,^p

11 mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi,

12 mfalme wa Egloni, mfalme wa Gezeri,^q

13 mfalme wa Debiri,^r mfalme wa Gederi,

14 mfalme wa Horma, mfalme wa Aradi,

15 mfalme wa Libna,^s mfalme wa Adulamu,

16 mfalme wa Makeda,^t mfalme wa Betheli,^u

17 mfalme wa Tapua, mfalme wa Heferi,

SURA YA 12

a Kum 29:7

b Yos 13:13

c Hes 21:26

d Hes 21:23, 24
Hes 21:33-35

e Hes 32:33
Kum 3:12, 13

f Yos 13:1, 5

g Yos 1:4

h Yos 11:16, 17

i Kum 2:12

j Yos 11:23

k Yos 10:40
Yos 11:16

l Mwa 15:16

m Kut 3:8
Kut 23:23
Kum 7:1

n Yos 6:2

o Yos 8:29

p Yos 10:23, 26

q Yos 10:33

r Yos 10:38

s Yos 10:29

t Yos 10:28

u Amu 1:22

Safu ya 2

a Yos 11:1, 10

b Yos 21:34

c Yos 11:1, 2

SURA YA 13

d Yos 23:1
Yos 24:29

e Kut 23:29, 30

f 1Sa 27:8

g Mwa 10:19

h Amu 3:1, 3
1Sa 6:4

i Yos 15:20, 46

j Amu 14:19

k 2Sa 21:19

l 1Sa 5:10

m Kum 2:23

n Amu 1:31

o 1Fa 5:18

18 mfalme wa Afeki, mfalme wa Lasharoni,

19 mfalme wa Madoni, mfalme wa Hasori,^a

20 mfalme wa Shimronmeroni, mfalme wa Akshafi,

21 mfalme wa Taanaki, mfalme wa Megido,

22 mfalme wa Kedeshi, mfalme wa Yokneamu^b kule Karmeli,

23 mfalme wa Dori kwenye miteremko ya Dori,^c mfalme wa Goimu kule Gilgali,

24 na mfalme wa Tirsa; jumla ya wafalme hao ni 31.

13 Basi Yoshua alikuwa amezeeka na umri wake ulikuwa umesonga sana.^d Kwa hiyo Yehova akamwambia, "Umezeeka na umri wako umesonga sana; na bado hamjamiliki* sehemu kubwa ya nchi. **2** Hii ndiyo nchi ambayo imebaki:^e maeneo yote ya Wafilisti na ya Wageshuri^f **3** (kuanzia kijito cha Mto Nile* kilicho upande wa mashariki wa^g Misri hadi kwenye mpaka wa Ekroni upande wa kaskazini, eneo lililoonwa kuwa sehemu ya Wakanaani)^g kutia ndani eneo la watawala watano wa Wafilisti^h—Wagaza, Waashdodi,ⁱ Waashkeloni,^j Wagathi,^k Waekroni;^j eneo la Waavimu^m **4** upande wa kusini; nchi yote ya Wakanaani; Meara, ambayo ni ya Wasidoni,ⁿ hadi Afeki, kwenye mpaka wa Waamori; **5** nchi ya Wagebali^o na nchi yote ya Lebanoni kuelekea mashariki, kuanzia Baalgadi chini ya Mlima Hermoni

13:1 * Au "hamjateka." **13:3** * Au "kijito cha Shihori." ^a Au "mbele ya."

hadi Lebo-hamathi;*^a **6** wa-kaaji wote wa eneo lenye milima kuanzia Lebanoni^b hadi Misrefoth-maimu;^c na Wasidoni wote.^d Nitawafukuza* mbele ya Waisraeli.^e Utaigawanya nchi hiyo na kuwapa Waisraeli kuwa urithi wao, kama nilivyokuamuru.^f **7** Na sasa yagawie makabila tisa pamoja na nusu ya kabila la Manase nchi hii kuwa urithi wao.*^g

8 Nusu iliyobaki ya kabila la Manase, pamoja na watu wa kabila la Rubeni na Gadi walichukua urithi wao waliope-wa na Musa upande wa mashariki wa Yordani, kama tu Musa mtumishi wa Yehova alivyowapa.^h **9** kuanzia Aroeri,ⁱ kwenye ukingo wa Bonde* la Arnoni,^j na jiji lililo katikati ya bonde hilo, na uwanda wote wa juu wa Medeba hadi Diboni; **10** na majiji yote ya Mfalme Sihoni wa Waamori, aliyetawala Heshboni, hadi kwenye mpaka wa Waamoni;^k **11** pia Gileadi na eneo la Wageshuri na Wamaakathi^l na eneo lote la Mlima Hermoni na Bashani^m hadi Saleka;ⁿ **12** ufalme wote wa Ogu kule Bashani, aliyetawala Ashtarothi na Edrei. (Alikuwa kati ya Warefaimu waliobaki.)^o Musa aliwashinda na kuwafukuza.*^p **13** Lakini Waisraeli hawakuwafukuza*^q Wageshuri na Wamaakathi, kwa kuwa Wageshuri na Wamaakathi wanaishi miongoni mwa Waisraeli mpaka leo.

14 Musa hakuwapa watu wa kabila la Lawi urithi.^r Urithi wao ni dhabihu zinazocho-

13:5 *Au "njia ya kuingia Hamathi."
13:6 *Au "Nitachukua nchi yao." 13:9,
16 *Au "Korongo." 13:12 *Au "kuchukua nchi yao." 13:13 *Au "hawakuchukua nchi ya."

SURA YA 13

a Hes 34:2, 8

b Kum 3:25

c Yos 11:8

d Amu 3:1-3

e Kut 23:30

f Hes 34:17
Yos 14:1

g Hes 33:54

h Hes 32:33
Yos 22:4

i Kum 3:12

j Hes 21:13

k Hes 21:23, 24

l Kum 3:14

m Yos 17:1

n 1Nya 5:11

o Kum 3:11

p Hes 21:23, 24
Hes 21:33-35q Hes 33:55
Yos 23:12, 13r Hes 18:20
Kum 10:9
Kum 12:12

Safu ya 2

a Law 7:33-35
Kum 18:1

b Hes 18:24

c Hes 21:25, 26

d Hes 32:37, 38

e Hes 21:23

f Kum 2:26

g Yos 21:8, 37

h Hes 32:37, 38

i Kum 3:16, 17

j Hes 33:48, 49

k Hes 21:25

l Kum 2:30

m Hes 31:7, 8

n Hes 22:5
2Pe 2:15

o Hes 22:7

p Hes 32:34, 35

q Yos 12:2
Amu 11:13

r 2Sa 11:1

s Hes 21:26

mwa kwa moto zinazotolewa kwa Yehova Mungu wa Israeli,^a kama alivyowaahidi.^b

15 Ndipo Musa akawapa urithi watu wa kabila la Rubeni kulingana na koo zao, **16** na eneo lao lilianza Aroeri, kwenye ukingo wa Bonde* la Arnoni, na jiji lililo kati-kati ya bonde hilo, na uwanda wote wa juu wa Medeba; **17** Heshboni na miji yake yote^c iliyo kwenye uwanda wa juu, Diboni, Bamoth-baali, Beth-baal-meoni,^d **18** Yahazi,^e Kedemothi,^f Mefaathi,^g **19** Kiriathaimu, Sibma,^h na Sereth-shahari kwenye mlima wa bondeni,* **20** Beth-peori, miteremko ya Pisga,ⁱ Beth-yeshimothi,^j **21** majiji yote kwenye uwanda wa juu, na eneo lote la Mfalme Sihoni wa Waamori, aliyetawala Heshboni.^k Musa alimshinda yeye^l pamoja na wakuu wa Midiani, yaani, Evi, Rekemu, Suri, Huru, na Reba,^m watawala vibaraka* wa Sihoni walio-kaa nchini humo. **22** Waisraeli walimuua kwa upanga Balaamuⁿ mwana wa Beori, yule mbashiri,*^o pamoja na watu wengine. **23** Na mpaka wa kabila la Rubeni ulikuwa Yordani; na eneo hilo lilikuwa urithi wa kabila la Rubeni kulingana na koo zao, pamoja na miji na vijiji vyake.

24 Pia, Musa akawapa urithi watu wa kabila la Gadi, kulingana na koo zao, **25** na eneo lao lilitia ndani Yazeri^p na majiji yote ya Gileadi na nusu ya nchi ya Waamoni^q hadi Aroeri, mbele ya Raba;^r **26** na kutoka Heshboni^s hadi

13:19 *Au "nchi tambarare ya chini."
13:21 *Yaani, wafalme waliokuwa chini ya Sihoni. 13:22 *Au "mwaguzi."

Ramath-mispe na Betonimu, na kutoka Mahanaimu^a hadi mpaka wa Debiri; **27** na bondoni,^b Beth-haramu, Beth-nimra,^b Sukothi,^c na Safoni, eneo lililobaki la Mfalme Sihoni wa Heshboni,^d na Mto Yordani ulikuwa mpaka ulioanzia upande wa chini wa Bahari ya Kinerethi,^e upande wa mashariki wa Yordani. **28** Huo ndio ulikuwa urithi wa kabila la Gadi kulingana na koo zao, pamoja na miji na vijiji vyake.

29 Pia, Musa akawapa urithi nusu ya watu wa kabila la Manase, ukawa urithi wao kulingana na koo zao.^f **30** Na eneo lao lilianzia Mahanaimu^g na eneo lote la Bashani, eneo lote la Mfalme Ogu wa Bashani, na vijiji vyote vya mahe-ma vya Yairi^h kule Bashani, miji 60. **31** Na nusu ya eneo la Gileadi, na Ashtarothi na Edrei,ⁱ majiji ya ufalme wa Ogu kule Bashani, yalichukuliwa na wana wa Makiri^j mwana wa Manase, yaani, nusu ya wana wa Makiri kulingana na koo zao.

32 Huo ndio urithi ambao Musa aliwapa katika mae-neo tambarare ya jangwani ya Moabu ng'ambo ya Yordani, upande wa mashariki wa Yeriko.^k

33 Lakini Musa hakuwapa urithi watu wa kabila la Lawi.^l Yehova Mungu wa Israeli ndiye urithi wao, kama alivyowaahidi.^m

14 Basi huu ndio urithi ambao kuhani Eleazari, Yoshua mwana wa Nuni, na viongozi wa koo* za makabi-

13:27 *Au "nchi tambarare ya chini."
^aYaani, Ziwa Genesareti, au Bahari ya Galilaya. **14:1** *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 13

- a Mwa 32:2
 Yos 21:8, 38
 b Hes 32:34, 36
 c Mwa 33:17
 d Hes 21:26
 e Hes 34:2, 11
 Kum 3:16, 17
 Yoh 6:1
 f Kum 3:13
 g 1Nya 6:77, 80
 h Hes 32:40, 41
 Kum 3:14
 i Hes 21:33
 j Hes 32:39
 k Hes 32:33
 l Kum 10:9
 Yos 18:7
 m Hes 18:24
 Hes 26:62, 63
 Kum 18:1

Safu ya 2

SURA YA 14

- a Hes 34:17
 Yos 19:51
 b Hes 26:55
 Hes 33:54
 Met 16:33
 Mdo 13:19
 c Hes 34:13
 d Hes 32:29
 e Kum 10:9
 Yos 13:14
 f Mwa 48:5
 1Nya 5:2
 g Mwa 48:19, 20
 h Hes 35:7
 Yos 21:1, 2
 i Hes 35:2, 5
 j Yos 4:19
 Yos 10:43
 k Hes 32:11, 12
 l Kum 1:35, 36
 m Hes 12:7, 8
 n Hes 13:26
 o Hes 13:2, 6
 p Hes 13:30
 Hes 14:6, 7
 q Hes 14:24
 Hes 32:11, 12

la ya Israeli waliwapa Waisraeli katika nchi ya Kanaani.^a **2** Waligawiwa urithi wao kwa kura,^b kama Yehova alivyomwagiza Musa aya-gawie yale makabila tisa na nusu.^c **3** Musa alikuwa tayari ameyapa makabila mawili na nusu urithi ng'ambo ya* Yordani,^d lakini hakuwapa Walawi urithi kati yao.^e **4** Wazao wa Yosefu walihesabiwa kuwa makabila mawili,^f Manase na Efraimu;^g nao hawakuwagawia Walawi urithi nchini, isipokuwa majiji^h ya kuishi na malisho kwa ajili ya mifugo yao na mali zao.ⁱ **5** Basi, Waisraeli aliigawanya nchi kama Yehova alivyomwamuru Musa.

6 Ndipo watu wa kabila la Yuda wakaenda kwa Yoshua kule Gilgali,^j na Kalebu^k mwana wa Yefune Mkenizi akamwambia: "Unajua vizuri maneno ambayo Yehova alimwambia Musa^l mtumishi wa Mungu wa kweli^m juu yangu na juu yako kule Kadesh-barnea.ⁿ **7** Nilikuwa na umri wa miaka 40 Musa mtumishi wa Yehova aliponituma kutoka Kadesh-barnea kwenda kuipeleleza nchi,^o nami nikamletea habari ya kweli.^p **8** Ingawa ndugu zangu walioenda pamoja nami waliwavunja watu moyo,^q mimi nilimfuata Yehova Mungu wangu kwa moyo wote.^q **9** Siku hiyo, Musa aliapa hivi: 'Nchi ambayo mguu wako umekanyaga itakuwa urithi wako na wa wana wako milele, kwa sababu umemfuata Yehova Mungu wangu kwa

14:3 *Yaani, upande wa mashariki wa.
 14:7 *Tnn., "neno kama lilivyokuwa moyoni mwangu."
 14:8 *Tnn., "walifanya moyo ya watu iyeyuke."
 *Tnn., "kika-milifu; kabisa."

moyo wote.^a **10** Basi kama alivyoahidi,^b Yehova amenihifadhi hai^c kwa miaka 45 tangu Yehova alipompa Musa ahadi hiyo Waisraeli walipotembea nyikani,^d ningali hai leo, nina umri wa miaka 85. **11** Lakini bado nina nguvu nilizokuwa nazo siku ambayo Musa alinituma. Bado nina nguvu nilizokuwa nazo wakati huo za kupigana vitani na kufanya kazi nyingine. **12** Kwa hiyo, nipe eneo hili lenye milima ambalo Yehova aliahidi siku hiyo. Ingawa ulisikia siku hiyo kwamba kuna Waanaki^e wanaoishi huko katika majiji makubwa yenye ngome,^f bila shaka* Yehova atakuwa pamoja nami,^g nami nitawafukuza,^h kama Yehova alivyoahidi.”^h

13 Ndipo Yoshua akambariki Kalebū mwana wa Yefune na kumpa Hebroni kuwa urithi wake.ⁱ **14** Ndiyo sababu Hebroni limekuwa urithi wa Kalebū mwana wa Yefune Mkenizi mpaka leo, kwa sababu alimfuata Yehova Mungu wa Israeli kwa moyo wote.^j **15** Hapo awali Hebroni liliitwa Kiriath-arba^k (Arba alikuwa mtu maarufu miongoni mwa Waanaki). Nchi ikawa na amani bila vita.^l

15 Nchi ambayo watu wa kabila la Yuda waligawiwa*^m kwa ajili ya koo zao ilifika kwenye mpaka wa Edomu,ⁿ nyika ya Zini, hadi upande wa kusini kabisa wa Negebu. **2** Mpaka wao wa kusini ulianza mwisho wa Bahari ya Chumvi,^o yaani, kuanzia mahali ambapo mto unai-

SURA YA 14

- a Kum 1:36
b Yos 21:45
c Hes 14:29, 30
d Hes 14:33
e Hes 13:33
f Hes 13:22, 28
g Hes 14:8
Ro 8:31
h Yos 15:14
Amu 1:20
i Yos 10:36, 37
Yos 15:13
Yos 21:11, 12
1Nya 6:55, 56
j Hes 14:24
Kum 1:35, 36
Yos 14:8
k Mwa 23:2
l Law 26:6
Yos 11:23

SURA YA 15

- m Hes 26:55
n Mwa 36:19
o Hes 34:2, 3

Safu ya 2

- a Amu 1:36
b Hes 34:4
c Hes 34:2, 5
d 1Fa 8:65
e Hes 34:12
f Yos 18:19, 20
g Yos 18:21, 22
h Yos 18:17, 20
i Yos 7:26
j Yos 5:8, 9
k Yos 18:17, 20
l 1Fa 1:9
m Yos 18:16, 20
2Fa 23:10
Yer 7:31
n Amu 1:21
o Yos 18:28
Amu 19:10

ngia baharini upande wa kusini. **3** Na uliendelea upande wa kusini kwenye mwinuko wa Akrabimu,^a ukavuka hadi Zini, na kupanda kutoka kusini hadi Kadesh-barnea,^b kufika Hezroni, Adari, na kuzunguka hadi Karka. **4** Kisha ukaendelea hadi Asimoni^c na kufika kwenye Korongo la Misri,^d nao ukafikia mwisho kwenye Bahari.* Huo ndio uliokuwa mpaka wao wa kusini.

5 Mpaka wa mashariki ulianza kwenye Bahari ya Chumvi hadi mahali ambapo Mto Yordani unaingia katika Bahari ya Chumvi, na mpaka wa kaskazini ulianza mahali ambapo Mto Yordani unaingia katika Bahari ya Chumvi.^e **6** Mpaka huo ulipanda hadi Beth-hogla^f na kuvuka upande wa kaskazini wa Beth-araba,^g nao uliendelea juu mpaka kwenye jiwe la Bohani^h mwana wa Rubeni. **7** Na mpaka huo ukapanda hadi Debiri katika Bonde la* Akoriⁱ na kugeuka kuelekea kaskazini hadi Gilgali,^j mbele ya njia inayopanda kuelekea Adumimu, ambayo iko upande wa kusini wa bonde la mto, kisha ukaendelea hadi kwenye chemchemi ya Enshemeshi^k na kufikia mwisho kule En-rogeli.^l **8** Na mpaka huo ukapanda hadi Bonde la Mwana wa Hinomu^m kwenye mteremko wa jiji la Wayebusiⁿ upande wa kusini, yaani, Yerusalemu,^o nao ukapanda hadi juu ya mlima unaotazamana na Bonde la Hinomu upande wa magharibi, yaani, mwisho kabisa wa Bonde la* Refaimu upande wa kaskazini. **9** Mpa-

14:12 *Au "inaelekea." #Au "nitachukua nchi yao." 15:1 *Au "waligawiwa kwa kura."

15:4 *Yaani, Bahari Kuu, Mediterania. 15:7, 8 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

ka huo ulianza juu ya mlima hadi chemchemi ya Neftoa^a mpaka kwenye majiji ya Mlima Efroni; nao ulifika Baala, yaani, Kiriath-yearimu.^b **10** Kisha ukazunguka kutoka Baala kuelekea upande wa magharibi hadi Mlima Seiri, ukaendelea hadi kwenye mteremko wa Mlima Yearimu upande wa kaskazini, yaani, Kesaloni, nao ukashuka hadi Beth-shemesh^c na kuendelea hadi Timna.^d **11** Kisha ukaendelea hadi kwenye mteremko wa kaskazini wa Ekroni,^e hadi Shikeroni, kufika kwenye Mlima Baala na kuendelea hadi Yabneeli, nao ulifikia mwisho kwenye bahari.

12 Mpaka wa magharibi ulikuwa Bahari Kuu*^f na pwani yake. Hiyo ndiyo iliyokuwa mipaka yote ya wazao wa Yuda kulingana na koo zao.

13 Naye Yoshua akampa Kalebu^g mwana wa Yefune sehemu ya nchi kati ya wazao wa Yuda kama Yehova alivyomwagiza Yoshua, yaani, eneo la Kiriath-arba (Arba alikuwa baba ya Waanaki), yaani, Hebroni.^h **14** Basi Kalebu aliwafukuza kutoka Hebroni wana watatu wa Anaki:ⁱ She-shai, Ahimani, Talmi,^j yaani, wazao wa Anaki. **15** Kisha akapanda kutoka huko na kwenda kuwashambulia wakaaji wa Debiri.^k (Hapo awali Debiri lilitwa Kiriath-seferi.) **16** Ndipo Kalebu akasema: "Yeyote atakayeshambulia na kuteka jiji la Kiriath-seferi, nitampa binti yangu Aksa awe mke wake." **17** Othnieli^l mwana wa Kenasi,^m ndugu ya Kalebu, akaliteka. Kwa

15:12 *Yaani, Mediterania.

SURA YA 15

a Yos 18:15, 20

b Yos 9:16, 17
2Sa 6:2
1Nya 13:6

c Yos 21:8, 16

d Yos 19:43, 48
Amu 14:1, 2
2Nya 28:16

e 1Sa 5:10
1Sa 7:14
2Fa 1:2

f Hes 34:2, 6
Kum 11:24

g Hes 13:30
Kum 1:36

h Mwa 23:2
Mwa 35:27
Yos 20:7
Yos 21:11, 12

i Hes 13:33
Yos 11:21

j Hes 13:22
Amu 1:10, 20

k Yos 10:38, 39

l Amu 3:9-11

m 1Nya 4:13

Safu ya 2

a 1Nya 2:49

b Amu 1:14, 15

c Hes 34:2, 3
Kum 2:5

d Yos 19:1, 2

e Ne 11:25, 26

f Mwa 21:31
Yos 19:1-3

g Hes 14:44, 45
Yos 19:1, 4
Amu 1:17

h Yos 19:1, 5
1Sa 27:5, 6
1Nya 12:1

i Yos 19:1, 7
Ne 11:25, 29

j Amu 1:9

k Yos 19:40, 41
Amu 16:31

l 1Sa 22:1

m 1Sa 17:1

n 1Sa 17:52

hiyo akampa Aksa^a binti yake awe mke wake. **18** Mwana-mke huyo alipokuwa akienda nyumbani kwake, akamsihi mume wake amwombe baba* yake shamba. Kisha mwana-mke huyo akashuka kutoka juu ya punda wake.[#] Kalebu akamuuliza: "Unataka nini?"^b **19** Akamwambia: "Tafadhali nibariki, kwa maana umeni-pia shamba upande wa kusini;* nipe pia Guloth-maimu."[#] Basi Kalebu akampa Gulothi ya Juu na Gulothi ya Chini.

20 Huo ndio uliokuwa urithi wa watu wa kabila la Yuda kulingana na koo zao.

21 Na majiji yaliyokuwa upande wa kusini kabisa wa kabila la Yuda kuelekea mpaka wa Edomu^c yalikuwa Kabzeeli, Ederi, Yaguri, **22** Kina, Dimona, Adada, **23** Kedeshi, Hasori, Ithnani, **24** Zifu, Telemu, Bealothi, **25** Hasor-hadata, na Kerioth-hesroni, yaani, Hasori, **26** Amamu, Shema, Molada,^d **27** Hasar-gada, Heshmoni, Beth-peleti,^e **28** Hasar-shuali, Beer-sheba,^f Biziothia, **29** Baala, limu, Esemu, **30** Eltoladi, Kesili, Horma,^g **31** Siklagi,^h Madmana, Sansana, **32** Lebaothi, Shilhimu, Aini, na Rimoniⁱ—jumla ya majiji 29, pamoja na vijiji vyake.

33 Majiji yaliyokuwa Shefela^j yalikuwa Eshtaoli, Sora,^k Ashna, **34** Zanoa, Enganimu, Tapua, Enamu, **35** Yarmuthi, Adulamu,^l Soko, Azeka,^m **36** Shaaraimu,ⁿ Adithaimu, na Gedera, na

15:18 *Yaani, "baba ya Aksa." [#]Au labda, "akapiga makofi akiwa juu ya punda ili kumwita baba yake." 15:19 *Au "eneo la Negebu." [#]Yaani, "Chemchemi za Maji."

Gederothaimu*—majiji 14 na vijiji vyake.

37 Senani, Hadasha, Migdal-gadi, **38** Dileani, Misphe, Yoktheeli, **39** Lakishi,^a Boskathi, Egloni, **40** Kaboni, Lahmamu, Kitilishi, **41** Gederothi, Beth-dagoni, Naama, na Makeda^b—majiji 16 na vijiji vyake.

42 Libna,^c Etheri, Ashani,^d **43** Ifta, Ashna, Nesibu, **44** Keila, Akzibu, na Maresha—majiji tisa na vijiji vyake.

45 Ekroni na miji na vijiji vyake; **46** kuanzia Ekroni kuelekea magharibi, miji yote iliyo kando ya Ashdodi na vijiji vyake.

47 Ashdodi,^e miji na vijiji vyake; Gaza,^f miji na vijiji vyake, hadi kwenye Bonde la Misri, na Bahari Kuu,* na eneo jirani.^g

48 Na katika eneo lenye milima, Shamiri, Yatiri,^h Soko, **49** Dana, Kiriath-sana, yaani, Debiri, **50** Anabu, Eshtemo,ⁱ Animu, **51** Gosheni,^j Holoni, na Gilo^k—majiji 11 na vijiji vyake.

52 Arabu, Duma, Eshani, **53** Yanimu, Beth-tapua, Afe-ka, **54** Humta, Kiriath-arba, yaani, Hebroni,^l na Siori—majiji tisa na vijiji vyake.

55 Maoni,^m Karmeli, Zifu,ⁿ Yuta, **56** Yezreeli, Yokdeamu, Zanoa, **57** Kayini, Gibea, Timna^o—majiji kumi na vijiji vyake.

58 Halhuli, Beth-suri, Gedor, **59** Maarathi, Beth-anothi, na Eltekoni—majiji sita na vijiji vyake.

15:36 *Au labda, "Gedera na mazizi yake ya kondoo." 15:47 *Yaani, Mediterania.

SURA YA 15

a 2Fa 18:14

b Yos 10:28

c Yos 10:29
2Fa 8:22

d Yos 19:1,7

e 1Sa 5:1

f Mwa 10:19

g Hes 34:2,5

h Yos 21:8,14

i 1Nya 6:57

j Yos 11:16

k 2Sa 15:12

l Yos 14:15

m 1Sa 23:25
1Sa 25:2,3

n 1Sa 23:14

o Mwa 38:12

Safu ya 2

a Yos 9:16,17
Yos 18:11,14
1Sa 7:1

b Yos 18:21,22

c 1Sa 23:29

d Hes 33:55
Amu 1:8,21
Amu 19:11
2Sa 5:6

e Mwa 10:15,16

f 1Nya 11:4

SURA YA 16

g Mwa 49:22
Kum 33:13h Hes 26:55
Hes 33:54
Met 16:33

i Yos 18:11,13

j Yos 18:11,13
1Nya 7:24

k 1Nya 7:20,28

l Mwa 48:5

m Kum 33:13-15
Yos 17:17,18

n Yos 18:11,13

o 2Nya 8:1,5

p Yos 17:7

60 Kiriath-baali, yaani, Kiriath-yearimu,^a na Raba—majiji mwili na vijiji vyake.

61 Katika nyika, Beth-araba,^b Midini, Sekaka, **62** Nibshani, Jiji la Chumvi, na Engedi^c—majiji sita na vijiji vyake.

63 Lakini watu wa kabila la Yuda hawakuwafukuza^d Wayebusi^e waliokuwa wakikaa Yerusalemu,^f basi tangu wakati huo Wayebusi wanakaa Yerusalemu pamoja na watu wa kabila la Yuda.

16 Na nchi ambayo wazao wa Yosefu^g waligawiwa^{*h} ilianzia Yordani huko Yeriko hadi kwenye vijito vilivyopo upande wa mashariki wa Yeriko, na kupitia nyikani hadi Yeriko katika eneo lenye milima la Betheli.ⁱ **2** Ilianzia Betheli ambayo ni sehemu ya Luzi na kuendelea hadi kwenye mpaka wa Waarki huko Atarothi, **3** nayo ikashuka kwenda magharibi hadi kwenye mpaka wa Wayafleti kufikia mpaka wa Beth-horoni^j ya Chini na Gezeri,^k na kufika kwenye bahari.

4 Na wazao wa Yosefu,^l yaani, watu wa kabila la Manase na kabila la Efraimu, wakamiliki nchi yao.^m **5** Na huu ndio mpaka wa wazao wa Efraimu kulingana na koo zao: Mpaka wa urithi wao upande wa mashariki ulikuwa Atarothadari,ⁿ hadi Beth-horoni ya Juu,^o **6** na mpaka huo ulifika kwenye bahari. Mikmethathi^p ilikuwa upande wa kaskazini, na mpaka huo ulizunguka upande wa mashariki hadi Taanath-shilo, kuelekea upande wa mashariki hadi Yanoa. **7** Kisha ukashu-

16:1 *Au "waligawiwa kwa kura."

ka kutoka Yanoa hadi Atarothi na Naara na kupita Yeri-ko^a hadi Yordani. **8** Kutoka Tapua^b ukaelekea magharibi hadi kwenye Bonde la Kana, na kufika kwenye bahari.^c Huo ndio urithi wa kabila la Efraimu kulingana na koo zao; **9** na wazao wa Efraimu walikuwa pia na majiji yaliyozungukwa katikati ya urithi wa wazao wa Manase.^d

10 Lakini hawakuwafukuzi Wakanaani waliokuwa waki-kaa Gezeri,^e na tangu wakati huo Wakanaani wanaishi miongoni mwa wazao wa Efraimu^f wakifanya kazi za kulazimishwa.^g

17 Kisha watu wa kabila la Manase,^h mzaliwa wa kwanza wa Yosefu,ⁱ wakagawiwa nchi yao kwa kura.^j Makiri,^k mzaliwa wa kwanza wa Manase na baba ya Gileadi, alikuwa amepewa nchi ya Gileadi na Bashani^l kwa sababu alikuwa mwanajeshi hodari. **2** Wazao waliobaki wa Manase waligawiwa nchi yao kwa kura kulingana na koo zao, yaani, wana wa Abiezeri,^m wana wa Heleki, wana wa Asrieli, wana wa Shekemu, wana wa Heferi, na wana wa Shemida. Hao ndio wazao wa kiume wa Manase mwana wa Yosefu, kulingana na koo zao.ⁿ **3** Lakini Selofehadi^o mwana wa Heferi, mwana wa Gileadi, mwana wa Makiri, mwana wa Manase, hakuwa na watoto wa kiume ila mabinti, na majina ya mabinti hao yalikuwa: Mala, Noa, Hogla, Milka, na Tirsia. **4** Basi wakaja kwa kuhani Eleazari,^p Yoshua mwana wa Nuni, na wakuu na kuwaambia: "Yehova ndiye aliyemwamuru Musa atupe urithi mio-

SURA YA 16

a Yos 6:20, 26

b Yos 17:8

c Hes 34:2, 6

d Yos 17:9

e Amu 1:29

f Hes 33:52, 55

g Yos 17:13

SURA YA 17

h Mwa 41:51

Mwa 46:20
Mwa 48:17, 18

i Kum 21:17

j Hes 26:55

Hes 33:54
Met 16:33

k Mwa 50:23

Hes 26:29
1Nya 7:14

l Kum 3:13

Yos 13:31

m Amu 6:11

n Hes 26:29-32

o Hes 26:33

p Hes 27:1, 2

Hes 34:17
Yos 14:1

Safu ya 2

a Hes 27:7, 11

b Hes 36:6, 12

c Yos 13:29

d Yos 16:5, 6

e Yos 20:7

Yos 24:1
1Nya 6:66, 67

f Yos 16:8

g Yos 16:9

h Yos 16:8

i Hes 34:2, 6

j 2Fa 9:27

k Yos 12:7, 23

ngoni mwa ndugu zetu."^a Basi akawapa urithi kati ya ndugu za baba yao kwa agizo la Yehova.^b

5 Na watu wa kabila la Manase walipewa pia maeneo mengine kumi zaidi ya nchi ya Gileadi na Bashani, ng'ambo ya* Yordani,^c **6** kwa kuwa binti za Manase walipokea pia urithi pamoja na wanawe, na nchi ya Gileadi ikawa mali ya wazao waliobaki wa Manase.

7 Na mpaka wa Manase ulianza Asheri hadi Mikmethathi,^d mbele ya Shekemu,^e na kuendelea hadi upande wa kusini* wa nchi ya wakaaji wa En-Tapua. **8** Nchi ya Tapua^f ikawa ya Manase lakini mji wa Tapua uliokuwa kwenye mpaka wa nchi ya Manase ulikuwa wa wazao wa Efraimu. **9** Na mpaka huo ulishuka hadi kwenye Bonde la Kana, upande wa kusini wa bonde hilo. Watu wa kabila la Efraimu walikuwa na majiji miongoni mwa majiji ya kabila la Manase,^g na mpaka wa Manase ulikuwa upande wa kaskazini wa bonde la mto, nao ulifika kwenye bahari.^h **10** Upande wa kusini ulikuwa wa kabila la Efraimu, na upande wa kaskazini ulikuwa wa Manase, na mpaka wake ulikuwa bahari,ⁱ na mpaka wa kaskazini* ulifika kwenye eneo la Asheri na mpaka wa mashariki ulifika kwenye eneo la Isakari.

11 Katika maeneo ya Isakari na Asheri, watu wa kabila la Manase walipewa Beth-sheani na miji yake, Ibleamu^j na miji yake, Dori^k na miji yake,

17:5 *Yaani, upande wa mashariki wa. **17:7** *Tnn., "upande wa kulia." **17:10** *Yaani, mpaka wa watu wa kabila la Manase au eneo la Manase.

En-dori^a na miji yake, Taanaki^b na miji yake, Megido na miji yake, maeneo matatu yenye milima.

12 Lakini wazao wa Manase hawakumiliki majiji hayo; Wakanaani waliendelea kukaa katika nchi hiyo.^c **13** Waisraeli walipopata nguvu, waliwatumikisha Wakanaani,^d lakini hawakuwafukuza* wote.^e

14 Wazao wa Yosefu wakaumuuliza Yoshua: "Kwa nini umetupatia eneo moja tu kwa kura^f na sehemu moja kuwa urithi wetu? Tuko wengi sana kwa sababu Yehova ametubariki mpaka sasa."^g **15** Yoshua akawajibu: "Ikiwa ninyi ni wengi sana na eneo lenye milima la Efraimu^h haliwatoshi, pandeni msituni katika nchi ya Waperiziⁱ na Warefaimu,^j mkaufyeke msitu ili mpate makao huko." **16** Kisha wazao wa Yosefu wakasema: "Eneo lenye milima halitutoshi, na Wakanaani wote wanaokaa bondeni,* yaani, wale wanaokaa Beth-sheani^k na miji yake na wale wanaokaa katika Bonde la[#] Yezreeli,^l wana magari ya vita^m yenye miundu ya chuma."^Δ **17** Basi Yoshua akaiambia hivi nyumba ya Yosefu, yaani, kabila la Efraimu na Manase: "Ninyi ni wengi sana, nanyi mna nguvu nyingi. Hamtapata eneo moja tu."ⁿ **18** eneo lenye milima litakuwa lenu pia.^o Ingawa ni msitu, ufyekeni, utakuwa mwisho wa eneo lenu. Mtawafukuza Wakanaani, hata kama wana nguvu na wana magari ya vita yenye miundu ya chuma."^{Δp}

17:13 *Au "hawakuchukua nchi yao."
17:16 *Au "nchi tambarare ya chini."
17:16, 18 ^ΔTnn., "magari ya chuma."

SURA YA 17

- a 1Sa 28:7
b Yos 12:7, 21
c Amu 1:27
d Yos 16:10
Amu 1:30
2Ny 8:8
e Kut 23:33
Hes 33:55
Kum 20:16, 17
Yos 23:12, 13
Amu 1:28
f Hes 33:54
g Mwa 48:19
Hes 26:34, 37
h Yos 24:33
i Kut 3:2
j Mwa 15:18-20
k Yos 17:11
l Yos 19:17, 18
Amu 6:33
m Kum 20:1
Amu 1:19
n Yos 17:14
o Hes 33:53
Yos 20:7
Amu 4:5
p Kum 20:1
Kum 31:6
Yos 13:6
Met 21:31

Safu ya 2

SURA YA 18

- a Hes 14:8
Kum 7:22
Kum 33:29
b Yos 19:51
Yos 22:9
Amu 21:19
c 1Sa 1:3
1Sa 4:3
Zb 78:60
Yer 7:12
Mdo 7:44, 45
d Hes 33:53, 55
e Hes 34:13
Yos 19:51
f Yos 15:1
g Yos 16:1, 4
h Hes 26:55
Hes 33:54
Yos 14:2
Met 16:33
Mdo 13:19
i Hes 18:20
Yos 13:33
j Kum 10:9
Kum 18:1
k Kum 3:12, 13
l Yos 19:51
Amu 21:19

18 Baada ya kuitiisha nchi,^a Waisraeli wote wakakusanyika Shilo^b na kupiga hema la mkutano^c huko. **2** Lakini makabila saba ya Waisraeli bado hayakuwa yamegawiwa urithi wao. **3** Ndi-po Yoshua akawaambia Waisraeli: "Mtakawia mpaka lini kumiliki nchi ambayo Yehova Mungu wa mababu zenu amewapa?^d **4** Chagueni wanau-me watatu kutoka kila kabila ili niwatume; watazunguka katika nchi yote na kuchora ramani kulingana na urithi wao. Kisha wataniletea habari. **5** Wataigawanya nchi hiyo katika maeneo saba.^e Kabila la Yuda litabaki katika eneo lake upande wa kusini,^f na nyumba ya Yosefu itabaki katika eneo lake upande wa kaskazini.^g **6** Igawanyeni nchi katika maeneo saba na kuniletea ramani yake, nami nita-wapa urithi kwa kupiga kura^h mbele za Yehova Mungu wetu. **7** Lakini Walawi hawajapewa urithi kati yenu,ⁱ kwa sababu ukuhani wa Yehova ndio urithi wao;^j na tayari Gadi, Rubeni, na nusu ya kabila la Manase^k wamechukua urithi wao upande wa mashariki wa Yordani, ambao Musa mtumishi wa Yehova aliwapa."^l

8 Wanaume hao wakajitayarisha kwenda kuchora ramani ya nchi, naye Yoshua akawaambia hivi: "Nendeni mkazunguke katika nchi yote, mchore ramani yake na kuniletea habari, nami nitawapa urithi kwa kupiga kura mbele za Yehova hapa Shilo."ⁱ **9** Basi wanaume hao wakaenda, wakazunguka nchini na kucho-ra ramani yenye maeneo saba

kulingana na majiji, wakaandika habari hizo katika kitabu. Kisha wakarudi kwa Yoshua kambini huko Shilo. **10** Ndiyo Yoshua akapiga kura kwa ajili ya maeneo hayo mbele za Yehova.^a Kisha Yoshua akawagawia Waisraeli nchi kulingana na makabila yao.^b

11 Kabila la Benjamini liligawiwa urithi wao kwa kura kulingana na koo zao, walipewa urithi kati ya kabila la Yuda^c na wazao wa Yosefu.^d

12 Mpaka wao wa kaskazini ulianza Yordani, na kwenda kaskazini kwenye mteremko wa Yeriko^e na kupanda mlimani upande wa magharibi, hadi katika nyika ya Beth-aveni.^f

13 Kisha ukaendelea mpaka Luzi kwenye mteremko wa kusini wa Luzi, yaani, Betheli;^g nao ukashuka hadi Atarothadari^h kwenye mlima ulio upande wa kusini wa Beth-horoni ya Chini.ⁱ **14** Na mpaka huo uligeuka upande wa magharibi kuelekea kusini kutoka kwenye mlima unaotazamana na Beth-horoni upande wa kusini; nao ukafika Kiriath-baali, yaani, Kiriath-yearimu,^j jiji la Yuda. Huo ndio mpaka wa magharibi.

15 Mpaka wa kusini ulianza mwisho wa jiji la Kiriath-yearimu, na kuelekea upande wa magharibi; kisha ukafika kwenye chemchemi ya Neftoa.^k **16** Nao ulishuka hadi mwisho wa mlima unaotazamana na Bonde la Mwana wa Hinomu,^l upande wa kaskazini katika Bonde* la Refaimu,^m nao ukashuka upande wa kusini katika Bonde la Hinomu, kwenye mteremko wa Myebu-

SURA YA 18

a Met 16:33

b Hes 33:54
Mdo 13:19

c Yos 15:1

d Yos 16:1

e Yos 2:1
Yos 16:1

f Yos 7:2

g Mwa 28:18, 19

h Yos 16:5

i Yos 10:11
Yos 21:20, 22

j Yos 15:9

k Yos 15:9, 12

l Yos 15:8, 12
Yer 7:31
Yer 19:2
Mt 5:22

m Kum 2:11

Safu ya 2

a Yos 15:63

b Yos 15:7, 12
1Fa 1:9

c Yos 15:7, 12

d Kum 19:14

e Yos 15:6, 12

f Yos 15:6, 12

g Hes 34:12

h Yos 15:6, 12

i Mwa 12:8
1Fa 12:28, 29

j Yos 21:8, 17

k Yos 9:16, 17
1Fa 3:4

l 2Sa 21:14

m Yos 15:8, 12
1Nya 11:4
2Nya 3:1

n 1Sa 10:26

SURA YA 19

o Yos 18:6

p Mwa 46:10

q Mwa 49:5, 7

r Mwa 21:31
Mwa 26:32, 33
Yos 15:21, 28s Yos 15:21, 26
1Nya 4:28-31

t Yos 15:21, 28

si,^a na kufika En-rogei.^b

17 Kisha ulielekea kaskazini hadi En-shemeshi na kufika Gellilothi, mbele ya njia inayopanda kuelekea Adumimu,^c na kushuka kwenye jibe^d la Bohani^e mwana wa Rubeni. **18** Ukaendelea hadi kwenye mteremko wa kaskazini mbele ya Araba na kushuka hadi Araba. **19** Kisha ukaendelea hadi kwenye mteremko wa kaskazini wa Beth-hogla,^f na kufika katika ghuba ya kaskazini ya Bahari ya Chumvi^g upande wa kusini wa Yordani. Huo ndio uliokuwa mpaka wa kusini. **20** Na Mto Yordani ulikuwa mpaka wa mashariki. Huo ndio uliokuwa urithi wa wazao wa Benjamini kulingana na koo zao, na hiyo ndiyo mipaka yao yote.

21 Na majiji ya kabila la Benjamini kulingana na koo zao yalikuwa: Yeriko, Beth-hogla, Emek-kesisi, **22** Beth-araba,^h Semaraimu, Betheli,ⁱ **23** Avimu, Para, Ofra, **24** Kefar-amoni, Ofni, na Geba^j—majiji 12 na vijiji vyake.

25 Gibeoni,^k Rama, Beerothi, **26** Misper, Kefira, Mosa, **27** Rekemu, Irpeeli, Tarala, **28** Zela,^l Ha-elefu, Yebusi, yaani, Yerusalemu,^m Gibeai,ⁿ na Kiriathi—majiji 14 na vijiji vyake.

Huo ndio uliokuwa urithi wa wazao wa Benjamini kulingana na koo zao.

19 Kura ya pili^o ilikuwa ya Simeoni, kwa ajili ya kabila la Simeoni^p kulingana na koo zao. Nao walipewa urithi kati ya urithi wa kabila la Yuda.^q **2** Urithi wao ulikuwa Beer-sheba,^r Sheba, Molada,^s **3** Hasar-shuali,^t Bala,

Esemu,^a **4** Eltoladi,^b Bethuli, Horma, **5** Siklagi,^c Bethmarkabothi, Hasar-susa, **6** Beth-lebaothi,^d na Sharuheni—majiji **13** na vijiji vyake; **7** Aini, Rimoni, Etheri, na Ashani^e—majiji manne na vijiji vyake; **8** na vijiji vyote vilivyozunguka majiji hayo mpaka Baalath-beeri, Rama ya kusini. Huo ndio uliokuwa urithi wa kabila la Simeoni kulingana na koo zao. **9** Kabila la Yuda lilikuwa na eneo kubwa sana, basi wazao wa Simeoni waligawiwa sehemu ya eneo hilo. Hivyo wazao wa Simeoni walipata urithi katikati ya kabila la Yuda.^f

10 Kura ya tatu^g ilikuwa ya wazao wa Zabuloni^h kulingana na koo zao, na mpaka wa urithi wao ulifika Saridi. **11** Mpaka wao ulipanda upande wa magharibi kuelekea Mareali kufika Dabeshethi na kuingia bondeni* mbele ya Yokneamu. **12** Na kutoka Saridi, ulielekea upande wa mashariki, na kufika kwenye mpaka wa Kisloth-tabori na kuendelea hadi Daberrathiⁱ na kupanda hadi Yafia. **13** Kisha ukaelekea mashariki hadi Gath-heferi^j na kufika Eth-kazini, hadi Rimoni, na kufika Nea. **14** Na mpaka huo uligeuka kuelekea Hanathoni upande wa kaskazini, na kufika kwenye Bonde la Iftaheli, **15** na Katathi, Nahalali, Shimroni,^k Idala, na Bethlehemu^l—majiji **12** na vijiji vyake. **16** Huo ndio uliokuwa urithi wa wazao wa Zabuloni kulingana na koo zao.^m Hayo ndiyo yaliyokuwa majiji na vijiji vyake.

19:11 *Au "korongoni."

SURA YA 19

a Yos 15:20, 29

b Yos 15:21, 30

c Yos 15:21, 31
1Sa 27:6

d Yos 15:21, 32

e Yos 15:20, 42
1Nya 4:24, 32
1Nya 6:59, 64

f Amu 1:3

g Yos 18:6

h Mwa 49:13

i Yos 21:27, 28

j 2Fa 14:25

k Yos 12:7, 20

l Amu 12:8

m Hes 26:27

Safu ya 2

a Hes 33:54

b Mwa 49:14

c Yos 17:16
Amu 6:33
1Fa 21:1

d 1Sa 28:4
1Fa 1:3
2Fa 4:8

e Yos 21:8, 29

f Amu 4:6

g Hes 26:25

h Hes 26:55
Yos 18:6

i Mwa 49:20

j Yos 21:8, 31

k 1Fa 18:19

l Mwa 10:15
Amu 1:31

m 2Sa 5:11
1Fa 5:1

n Amu 1:31

o Yos 21:8, 31

p Hes 26:47

q Hes 26:55
Yos 18:6

17 Kura ya nne^a ilikuwa ya Isakari,^b kwa ajili ya wazao wa Isakari kulingana na koo zao. **18** Na mpaka wao ulifika Yezreeli,^c Kesulothi, Shunemu,^d **19** Hafaraimu, Shioni, Anaharathi, **20** Rabithi, Kishioni, Ebesi, **21** Remethi, Enganimu,^e En-hada, na Bethpasesi. **22** Na mpaka huo ulifika Tabori^f na Shahasuma na Beth-shemeshi, na kufika kwenye Mto Yordani—majiji **16** na vijiji vyake. **23** Huo ndio uliokuwa urithi wa kabila la Isakari kulingana na koo zao,^g majiji na vijiji vyake.

24 Kura ya tano^h ilikuwa ya kabila la Asheriⁱ kulingana na koo zao. **25** Mpaka wao ulipita Helkathi,^j Hali, Beteni, Akshafi, **26** Alameleki, Amadi, na Mishali. Nao ulifika upande wa magharibi hadi Karmeli^k na kuelekea Shihorlibnathi, **27** nao uligeuka na kuelekea Beth-dagoni upande wa mashariki na kufika Zabuloni na Bonde la Iftah-eli upande wa kaskazini, hadi Bethemeki na Neieli, kisha ukaelekea Kabuli upande wa kushoto, **28** na Ebroni, Rehobu, Hamoni, na Kana hadi Sidoni Kuu.^l **29** Na mpaka huo ukageuka kurudi Rama na kufika kwenye jiji la Tiro lenye ngome.^m Kisha ukageuka kurudi Hosa, na kufika kwenye bahari katika eneo la Akzibu, **30** Uma, Afeki,ⁿ na Rehobu^o—majiji **22** na vijiji vyake. **31** Huo ndio uliokuwa urithi wa kabila la Asheri kulingana na koo zao.^p Hayo ndiyo yaliyokuwa majiji na vijiji vyake.

32 Kura ya sita^q ilikuwa ya wazao wa Naftali, kwa ajili ya wazao wa Naftali kulingana na koo zao. **33** Mpa-

ka wao ulianza Helefu, kuto-ka kwenye mti mkubwa kule Saanimu,^a kuelekea Adaminekebu na Yabneeli hadi Lakumu; na kufika kwenye Mto Yordani. **34** Na kutoka huko ukageuka na kuelekea magharibi hadi Aznoth-tabori na kwenda Hukkoki mpaka Zabuloni upande wa kusini na kupakana na Asheri upande wa magharibi na kuendelea hadi Yuda, na kufika kwenye Mto Yordani upande wa mashariki. **35** Na majiji yenye ngo-me yalikuwa Sidimu, Seri, Hamathi,^b Rakathi, Kinere-thi, **36** Adama, Rama, Hasori,^c **37** Kedeshi,^d Edrei, Enhasori, **38** Yironi, Migdaleli, Horemu, Beth-anathi, na Beth-shemeshi^e—majiji 19 na vijiji vyake. **39** Huo ndio uliokuwa urithi wa kabila la Naftali kulingana na koo zao,^f majiji na vijiji vyake.

40 Kura ya saba^g ilikuwa ya kabila la Dani^h kulingana na koo zao. **41** Na mpaka wa urithi wao ulipita Sora,ⁱ Eshtauli, Ir-shemeshi, **42** Shaalabini,^j Aiyaloni,^k Ithla, **43** Eloni, Timna,^l Ekroni,^m **44** Elteke, Gibethoni,ⁿ Baalathi, **45** Yehudi, Bene-beraki, Gath-rimoni,^o **46** Me-yarkoni, na Rakoni, mpaka ukiwa mbele ya Yopa.^p **47** Lakini eneo la kabila la Dani halikuwatoshwa kwa sababu lilikuwa dogo.^q Basi wakaenda kushambulia jiji la Leshemu,^r wakaliteka na kuwaangamiza wakaaji wake kwa upanga. Wakalimiliki na kukaa ndani yake, kisha wakabadili jina Leshemu kuwa Dani, jina la babu yao.^s **48** Huo ndio uliokuwa urithi wa kabila la Dani kulingana na

SURA YA 19

a Amu 4:11

b Yos 21:32

c Yos 11:10
Amu 4:2
ISA 12:9

d Yos 20:7

e Amu 1:33

f Hes 26:50

g Yos 18:6

h Mwa 49:17

i Yos 15:20, 33
Amu 13:2

j Amu 1:35

k Yos 10:12
Yos 21:8, 24

l Amu 14:1

m Yos 15:20, 45

n Yos 21:8, 23

o Yos 21:8, 24

p Yon 1:3
Mdo 9:36q Hes 26:54
Hes 33:54

r Amu 18:7

s Amu 18:29

Safu ya 2

a Yos 24:29, 30

b Hes 34:17
Yos 14:1c Amu 21:19
Yer 7:12

d Yos 18:1, 8

SURA YA 20

e Kut 21:12, 13
Hes 35:14, 15
Kum 4:41f Mwa 9:6
Kut 21:23
Hes 35:26, 27

g Kum 19:3

h Met 31:23

i Hes 35:22-24
Kum 19:4-6

koo zao. Hayo ndiyo yaliyoku-wa majiji na vijiji vyake.

49 Basi wakamaliza ku-gawanya nchi ya urithi ku-lingana na maeneo yake. Ki-sha Waisraeli wakampa Yoshua mwana wa Nuni urithi kati yao. **50** Kwa agizo la Yehova walimpa jiji ambalo aliomba, yaani, Timnath-sera,^a kati-ka eneo lenye milima la Efraimu, akalijenga upya na kukaa ndani yake.

51 Huo ndio urithi ambao kuhani Eleazari, Yoshua mwana wa Nuni, na viongozi wa koo* za makabila ya Waisraeli waligawanya^b kwa kura kule Shilo^c mbele za Yehova, kwenye mlango wa hema la mkutano.^d Basi wakamaliza ku-gawanya nchi.

20 Kisha Yehova akamwambia Yoshua: **2** "Wambie Waisraeli, 'Jichagulieni majiji ya makimbilio^e kama nilivyowaambia kupitia Musa, **3** ili mtu atakayemua mwenzake* bila kukusudia au bila kujua akim-bilie humo. Atakimbilia humo ili kumkwepa mtu anayetaka kulipiza kisasi cha damu.^f

4 Ni lazima akimbilie moja-wapo ya majiji hayo^g na kusimama langoni,^h kisha atawaambia wazee wa jiji hilo kesi yake. Nao lazima wampokee jijini na kumpa makao, naye ataishi pamoja nao.

5 Na yule anayetaka kulipiza kisasi cha damu akimfuatia, wazee hawapaswi kumtia muuaji huyo mikononi mwake, kwa maana alimua mwenzake bila kukusudia,* wala hakuwa akimchukia.ⁱ

19:51 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. **20:3** *Au "anayeya nafsi." **20:5** *Au "bila kujua."

6 Ni lazima akae ndani ya jiji hilo mpaka kesi yake itakaposikilizwa mbele ya kusanyiko,^a naye atabaki humo mpaka kuhani mkuu^b anayehudumu wakati huo atakapokufa. Kisha muuaji huyo anaweza kurudi nyumbani kwake katika jiji alilokimbia.”^c

7 Basi wakatenga majiji haya kuwa matakatifu: Kedeshi^d kule Galilaya katika eneo lenye milima la Naftali, Shekemu^e katika eneo lenye milima la Efraimu, na Kiriath-arba,^f yaani, Hebroni, katika eneo lenye milima la Yuda. 8 Na katika eneo la Yordani, upande wa mashariki wa Yeriko, wakachagua jiji la Beseri^g lililo nyikani kwenye uwanda wa juu katika eneo la kabila la Rubeni, Ramothi^h kule Gileadi katika eneo la kabila la Gadi, na Golaniⁱ kule Bashani katika eneo la kabila la Manase.^j

9 Hayo ndiyo majiji yaliyochaguliwa kwa ajili ya Waisraeli wote na wageni walioishi kati yao, ili mtu yeyote atakayemua mwenzake bila kukusudia akimbilie humo,^k ili asiuaawe na mtu anayetaka kupipiza kisasi cha damu mpaka kesi yake isikilizwe mbele ya kusanyiko.^l

21 Viongozi wa koo* za Walawi wakaenda kwa kuhani Eleazari^m na Yoshua mwana wa Nuni na viongozi wa koo* za makabila ya Israeli, 2 wakawaambia hivi huko Shiloⁿ katika nchi ya Kanaani: “Yehova aliamuru kupitia Musa tupewe majiji ya kuishi na malisho ya mifugo yetu.”^o 3 Basi kwa agizo la Yehova, Waisraeli wakawapa Walawi

21:1 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 20

a Hes 35:12, 24
b Hes 35:25
c Hes 35:28
d Yos 21:32
e Mwa 33:18
Yos 21:20, 21
f Yos 14:15
Yos 21:13
g Yos 21:8, 36
1Nya 6:77, 78
h Yos 21:8, 38
1Nya 6:77, 80
i Yos 21:27
1Nya 6:71
j Kum 4:41-43
k Hes 35:11, 15
l Hes 35:12, 24
Kum 21:5

SURA YA 21

m Hes 34:17
n Yos 18:1
o Law 25:33, 34
Hes 35:2-4
Yos 14:4

Safu ya 2

a Hes 35:8
b Mwa 49:5, 7
c Mwa 46:11
Hes 3:27-31
d 1Nya 6:54, 55
e Yos 19:1
f 1Nya 6:60, 64
g 1Nya 6:66
h 1Nya 6:61, 70
i Kut 6:17
Hes 3:21, 22
j Hes 32:33
1Nya 6:62
k Kut 6:19
l 1Nya 6:63
m Hes 35:2, 5
n 1Nya 6:64, 65
o Mwa 23:2
Mwa 35:27
Yos 15:13, 14
Yos 20:7
Amu 1:10
p 2Sa 2:1
2Sa 15:10
1Nya 6:54-56
q Amu 1:20
r Hes 35:6, 15

majiji hayo^a na malisho yake kutoka katika urithi wao wenyewe.^b

4 Kura ya kwanza ilikuwa ya koo za Wakohathi,^c na Walawi waliokuwa wazao wa kuhani Haruni walipewa majiji 13 kwa kura katika maeneo ya kabila la Yuda,^d kabila la Simeoni,^e na kabila la Benjamini.^f

5 Na Wakohathi waliobaki walipewa majiji kumi kwa kura katika maeneo ya koo za kabila la Efraimu,^g Dani, na katika eneo la nusu ya kabila la Manase.^h

6 Na Wagershoniⁱ walipewa majiji 13 kwa kura katika maeneo ya koo za kabila la Isakari, Asheri, Naftali, na katika eneo la nusu ya kabila la Manase kule Bashani.^j

7 Na Wamerari^k walipewa majiji 12 kulingana na koo zao katika maeneo ya kabila la Rubeni, Gadi, na Zabuloni.^l

8 Hivyo Waisraeli wakawapa Walawi majiji hayo na malisho yake kwa kura kama Yehova alivyokuwa ameamuru kupitia Musa.^m

9 Yafuatayo ni majina ya majijiⁿ katika maeneo ya kabila la Yuda na kabila la Simeoni ambayo waliwapa 10 wana wa Haruni wa koo za Walawi Wakohathi, kwa kuwa kura ya kwanza ilikuwa yao. 11 Waliwapa Kiriath-arba^o (Arba alikuwa baba ya Waanaki), yaani, jiji la Hebroni,^p katika eneo lenye milima la Yuda, na malisho yake yote. 12 Lakini walikuwa wamempa Kalebu mwana wa Yefune mashamba ya jiji hilo na vijiji vyake kuwa urithi wake.^q

13 Nao wakawapa wana wa kuhani Haruni jiji la makimbilio kwa ajili ya muuaji,^r

yaani, jiji la Hebroni,^a na malisho yake, pia Libna^b na malisho yake, **14** Yatiri^c na malisho yake, Eshtemoa^d na malisho yake, **15** Holoni^e na malisho yake, Debiri^f na malisho yake, **16** Aini^g na malisho yake, Yuta^h na malisho yake, na Beth-shemeshi na malisho yake—majiji tisa katika maeneo ya makabila hayo mawili.

17 Na katika eneo la kabila la Benjamini: Gibeoniⁱ na malisho yake, Geba na malisho yake,^j **18** Anathothi^k na malisho yake, na Almoni na malisho yake—majiji manne.

19 Wazao wa Haruni, makuhani, walipewa jumla ya majiji 13 na malisho yake.^l

20 Na Walawi waliobaki wa koo za Wakohathi walipewa majiji kwa kura katika eneo la kabila la Efraimu. **21** Waliwapa jiji la makimbilio kwa ajili ya muuaji,^m yaani, jiji la Shekemuⁿ na malisho yake katika eneo lenye milima la Efraimu, Gezeri^o na malisho yake, **22** Kibsaimu na malisho yake, na Beth-horoni^p na malisho yake—majiji manne.

23 Na katika eneo la kabila la Dani: Elteke na malisho yake, Gibethoni na malisho yake, **24** Aiyaloni^q na malisho yake, Gath-rimoni na malisho yake—majiji manne.

25 Na katika eneo la nusu ya kabila la Manase: Taanaki^r na malisho yake na Gath-rimoni na malisho yake—majiji mawili.

26 Koo zilizobaki za Wakohathi zilipewa jumla ya majiji kumi na malisho yake.

27 Na Wagershoni^s wa koo za Walawi walipewa jiji la ma-

SURA YA 21

a Yos 15:20, 54

b Yos 15:20, 42

c Yos 15:20, 48

d Yos 15:20, 50

e Yos 15:20, 51

f Yos 15:20, 49

1Nya 6:57, 58

g Yos 19:1, 7

h Yos 15:20, 55

i Yos 9:3

Yos 18:21, 25

j 1Nya 6:57, 60

k Yer 1:1

l Law 25:33, 34

Hes 35:4

m Hes 35:11, 15

n Yos 20:7

1Fa 12:1

o Yos 16:10

p Yos 16:1, 3

Yos 18:11, 13

q Yos 10:12

Amu 1:35

2Nya 28:18

r Yos 17:11

s Yos 21:6

Safu ya 2

a 1Nya 6:71

b 1Nya 6:72, 73

c Yos 19:12, 16

d 1Nya 6:74, 75

e Yos 19:25, 31

f Yos 19:28, 31

Amu 1:31

g Hes 35:14, 15

h Yos 20:7

i Yos 21:7

j Yos 19:10, 11

k 1Nya 6:77

l Amu 1:30

m Kum 4:41-43

Yos 20:8

n 1Nya 6:78, 79

o 1Nya 6:80, 81

p Yos 20:8, 9

1Fa 22:3

q Mwa 32:2

2Sa 2:8

r Hes 21:26

Hes 32:37

kimbilio kwa ajili ya muuaji katika eneo la nusu ya kabila la Manase, yaani, jiji la Golani^a kule Bashani pamoja na malisho yake, na Beeshtera na malisho yake—majiji mawili.

28 Na katika eneo la kabila la Isakari:^b Kishioni na malisho yake, Daberathi^c na malisho yake, **29** Yarmuthi na malisho yake, na Enganimu na malisho yake—majiji manne.

30 Na katika eneo la kabila la Asheri:^d Mishali na malisho yake, Abdoni na malisho yake, **31** Helkathi^e na malisho yake, na Rehobu^f na malisho yake—majiji manne.

32 Na katika eneo la kabila la Naftali: jiji la makimbilio^g kwa ajili ya muuaji, yaani, jiji la Kedeshi^h kule Galilaya na malisho yake, Hamoth-dori na malisho yake, na Kartani na malisho yake—majiji matatu.

33 Wagershoni walipewa jumla ya majiji 13 na malisho yake kulingana na koo zao.

34 Na koo za Wamerari,ⁱ yaani, Walawi waliobaki, walipewa Yokneamu^j na malisho yake, Karta na malisho yake, katika eneo la kabila la Zabuloni,^k **35** Dimna na malisho yake, na Nahalali^l na malisho yake—majiji manne.

36 Na katika eneo la kabila la Rubeni: Beseri^m na malisho yake, Yahazi na malisho yake,ⁿ **37** Kedemothi na malisho yake, na Mefaathi na malisho yake—majiji manne.

38 Na katika eneo la kabila la Gadi:^o jiji la makimbilio kwa ajili ya muuaji, yaani, jiji la Ramothi kule Gileadi^p na malisho yake, Mahanaimu^q na malisho yake, **39** Heshboni^r na

malisho yake, Yazeri^a na malisho yake—jumla ya majiji manne.

40 Majiji yote ambayo Wamerari walipewa kwa kura kulingana na koo zao, yaani, koo zilizobaki za Walawi, yalikuwa majiji 12.

41 Majiji yote ambayo Walawi walipewa katika maeneo ya Waisraeli yalikuwa majiji 48 pamoja na malisho yake.^b

42 Kila moja la majiji hayo lilizungukwa na malisho—hivyo ndivyo ilivyokuwa katika majiji hayo yote.

43 Basi Yehova akawapa Waisraeli nchi yote ambayo aliapa kwamba angewapa mababu zao,^c wakaimiliki na kuisi humo.^d **44** Yehova akawapa pia amani katika nchi yote, kama alivyowapa pia mababu zao,^e na hakuna adui hata mmoja kati ya maadui wao wote aliyeweza kuwashinda.^f Yehova aliwalia maadui wao wote mikononi mwao.^g **45** Hakuna ahadi hata moja iliyokosa kutimia kati ya ahadi zote nzuri ambazo Yehova aliwaahidi Waisraeli; zote zilitimia.^h

22 Kisha Yoshua akawaita watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase **2** na kuwaambia: “Mmefanya mambo yote ambayo Musa mtumishi wa Yehova aliwaamuru mfanye,ⁱ nanyi mmetii sauti yangu kwa kufanya mambo yote niliyowaamuru.^j **3** Hamjawaacha ndugu zenu kwa muda wote huo, mpaka leo hii,^k nanyi mmetimiza wajibu wa kushika amri ya Yehova Mungu wenu.^l **4** Na Yehova Mungu wenu amewapumzisha ndugu zenu kama alivyowaahidi.^m

SURA YA 21

a Hes 32:1

b Hes 35:5, 7

c Mwa 13:14, 15

Mwa 15:18

Mwa 26:3

Mwa 28:4

d Kut 23:30

e Kut 33:14

Kum 12:10

Yos 1:13

Yos 11:23

Yos 22:4

f Kum 28:7

g Kum 7:24

Kum 31:3

h Yos 23:14

1Fa 8:56

Ebr 6:18

SURA YA 22

i Hes 32:20–22

Kum 3:18

j Yos 1:16

k Yos 11:18

l Hes 32:25–27

m Yos 21:44

Safu ya 2

a Hes 32:33

b Kum 6:6

Kum 12:32

2Fa 21:8

c Kum 6:5

Kum 11:1

Mt 22:37

d Kum 10:12

e Kum 13:14

1Yo 5:3

f Kum 4:4

Kum 10:20

Yos 23:8

g Kum 6:13

Yos 24:15

Lu 4:8

h Kum 4:29

Kum 11:13

Mk 12:30, 33

i Yos 13:29, 30

j Yos 17:5

k Kum 28:8

l Hes 31:27

m Hes 32:1

n Hes 32:33

Basi sasa rudini kwenye mahema yenu katika nchi ambayo Musa mtumishi wa Yehova aliwapa ng'ambo ya* Yordani.^a **5** Lakini muwe waa-ngalifu sana kutekeleza amri na Sheria ambayo Musa mtumishi wa Yehova aliwapa,^b kwa kumpenda Yehova Mungu wenu,^c kutembea katika njia zake zote,^d kushika amri zake,^e kushikamana naye,^f na kumtumikia^g kwa moyo wenu wote na nafsi* yenu yote.”^h

6 Basi Yoshua akawabariki na kuwaambia waende zao, nao wakarudi katika mahema yao. **7** Musa alikuwa ameipa nusu ya kabila la Manase urithi kule Bashani,ⁱ na Yoshua akaipa nusu iliyobaki ya kabila hilo nchi upande wa magharibi wa Yordani,^j pamoja na ndugu zao. Zaidi ya hilo, Yoshua alipowaambia warudi katika mahema yao, aliwabariki **8** na kuwaambia: “Rudini katika mahema yenu mkiwa na utajiri mwingi, mifugo mingi sana, fedha na dhahabu, shaba na chuma, na mavazi mengi sana.^k Gawaneni na ndugu zenu nyara mlizochukua^l kutoka kwa maadui wenu.”

9 Kisha watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase wakawaacha Waisraeli wengine huko Shilo katika nchi ya Kanaani, wakarudi Gileadi,^m nchi yao ya urithi waliyokuwa wakiimiliki kama Yehova alivyowaagiza kupitia Musa.ⁿ **10** Watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase walipofika maeneo ya Yordani katika nchi ya Kanaani, walijenga

22:4 *Yaani, upande wa mashariki wa. **22:5** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

madhabahu karibu na Mto Yordani, madhabahu kubwa inayovutia. **11** Baadaye Waisraeli wengine wakasikia^a iki-semwa, “Watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase wamejenga madhabahu kwenye mpaka wa nchi ya Kanaani katika maeneo ya Yordani ambayo ni ya Waisraeli.” **12** Waisraeli waliposikia habari hizo, wakakusanyika wote Shilo^b ili waende kupigana nao.

13 Kisha Waisraeli wakamtuma Finehasi^c mwana wa kuhani Eleazari kwa watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase katika nchi ya Gileadi, **14** na wakuu kumi walikuwa pamoja naye, mkuu mmoja kwa ajili ya kila ukoo* katika makabila yote ya Israeli, kila mmoja wao alikuwa kiongozi wa ukoo wake* miongoni mwa maelfu ya^d Israeli. **15** Walipofika kwa watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase katika nchi ya Gileadi, wakawaambia:

16 “Kusanyiko lote la Yehova linasema hivi: ‘Mnawezaje kukosa uaminifu kwa Mungu wa Israeli kwa kufanya jambo kama hili?’^e Leo, mmeacha kumfuata Yehova kwa kujijengea madhabahu na kumwasi Yehova.^f **17** Je, dhambi tuliyotenda kule Peori haikutosha? Mpaka leo hatujajitakasa kutokana nayo hata ingawa kusanyiko la Yehova lilipata pigo.^g **18** Na sasa mnaacha kumfuata Yehova! Mkimwasi Yehova leo, kesho atawakasirikia Waisraeli wote.^h

22:14 * Yaani, ukoo wa upande wa baba.
^a Au “koo za.”

SURA YA 22

a Kum 13:12,15

b Yos 18:1
Yos 19:51c Kut 6:25
Hes 25:11
Amu 20:28d Hes 1:16
Kum 1:13

e Yos 22:11, 12

f Kum 12:13, 14

g Hes 25:3, 9
Kum 4:3h Yos 7:1
1Ny 21:14

Safu ya 2

a Hes 34:2
Yos 1:11

b Yos 18:1

c Kum 12:13, 14

d Yos 7:1

e Yos 7:11, 15

f Yos 7:5
Yos 7:24, 25

g Yos 22:13, 14

h Kum 10:17

i Kum 12:11, 13

19 Basi ikiwa mnaona nchi mliyorithi si safi, vukeni na kuingia katika nchi ya Yehova^a ambayo ina hema la ibada^b ya Yehova mkae kati yetu, lakini msimwasi Yehova, wala msitufanye tuwe waasi kwa kujijengea madhabahu nyingine zaidi ya madhabahu ya Yehova Mungu wetu.^c **20** Akani^d mwana wa Zera alipokosa uaminifu na kuchukua kitu kilichopaswa kuharibiwa, je, Mungu hakuwakasirikia Waisraeli wote?^e Akani hakufa peke yake kwa sababu ya dhambi yake.^f

21 Ndipo watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase wakawajibu hivi viongozi wa maelfu* katika Israeli:^g **22** “Mungu wa miungu, Yehova!* Mungu wa miungu, Yehova!^h Anajua, na Waisraeli pia watajua. Ikiwa tuliasi na kukosa uaminifu kwa Yehova, msituache hai leo. **23** Ikiwa tulijijengea madhabahu ili tuache kumfuata Yehova na kutoa juu yake dhambi za kuteketezwa, matoleo ya nafaka, na dhambi za ushirika, Yehova atatuadhibu.ⁱ **24** Lakini hatukuijenga kwa sababu hiyo, tulijenga kwa sababu tulisema, ‘Wakati ujao wana wenu watawauliza wana wetu: “Mna haki gani ya kumwabudu* Yehova Mungu wa Israeli? **25** Yehova ameweka Mto Yordani kuwa mpaka kati yetu na ninyi, watu wa kabila la Rubeni na Gadi. Hamna ushirika wowote na Yehova.” Na wana wenu watawazua wana wetu kumwabudu* Yehova.’

22:21 * Au “koo.” 22:22 * Au “Mungu Mkuu, Yehova.” 22:24 * Tnn., “Mna nini na.” 22:25 * Tnn., “kumwogopa.”

26 “Basi tukasema, ‘Kwa vyovyote vile, tujenge madhabahu, lakini si kwa ajili ya matoleo au dhabihu za kutekelezwa, **27** bali iwe ushahidi kati yetu na ninyi^a na wazao wetu* kwamba tutamtumikia Yehova kwa dhabihu zetu za kutekelezwa, na matoleo yetu, na dhabihu zetu za ushrika,^b ili wana wenu wasiwaambie hivi wana wetu wakati ujao: “Hamna ushirika wowote na Yehova.”” **28** Basi tukasema, ‘Wakituambia hivyo sisi na wazao wetu* wakati ujao, tutawajibu: “Angalieni mfano wa madhabahu ya Yehova ambayo mababu zetu walijenga, si kwa ajili ya matoleo au dhabihu za kutekelezwa, bali iwe ushahidi kati yetu na ninyi.”” **29** Hatuwezi kamwe kuwazia kumwasi Yehova na kuacha kumfuata^c Yehova kwa kujenga madhabahu nyingine kwa ajili ya dhabihu za kutekelezwa, matoleo ya nafaka, na matoleo mengine, zaidi ya madhabahu ya Yehova Mungu wetu ambayo iko mbele ya hema lake la ibada!”^d

30 Basi kuhani Finehasi, wakuu wa Waisraeli, na viongozi wa maelfu* katika Israeli waliokuwa pamoja naye waliposikia maneno yaliyosemwa na wazao wa Rubeni, Gadi, na Manase, wakaridhika.^e **31** Ndipo Finehasi mwana wa kuhani Eleazari akawaambia wazao wa Rubeni, Gadi, na Manase: “Leo tunajua kwamba Yehova yuko kati yetu kwa sababu hamjako-sa uaminifu kwa Yehova kati-ka jambo hili. Sasa mmewao-

22:27, 28 *Tnn., “vizazi vyetu.” 22:30 *Au “koo.”

SURA YA 22

a Mwa 31:48
Yos 24:27

b Kum 12:5,6

c Kum 6:14

d Kum 12:14

e Yos 22:13,14

Safu ya 2

SURA YA 23

a Kut 33:14
Law 26:6
Yos 21:44

b Yos 13:1

c Kum 31:28

d Kum 16:18

e Kum 20:4
Yos 10:11-14
Yos 10:40,42

f Yos 18:10

g Kum 7:1

h Yos 13:2-6

koa Waisraeli kutoka mikononi mwa Yehova.”

32 Baada ya Finehasi mwana wa kuhani Eleazari na wale wakuu kukutana na watu wa kabila la Rubeni na Gadi katika nchi ya Gileadi wakarudi katika nchi ya Kanaani na kuwaambia Waisraeli wengine habari hizo. **33** Na Waisraeli wakaridhika na habari hizo. Wakamsifu Mungu na kuacha mipango ya kupigana na watu wa kabila la Rubeni na Gadi na kuiharibu nchi yao.

34 Watu wa kabila la Rubeni na Gadi wakaipa jina madhabahu* hiyo, kwa sababu walisema “ni ushahidi kati yetu kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli.”

23 Siku nyingi baada ya Yehova kuwapa Waisraeli amani^a kwa kuwaokoa kutoka kwa maadui wote waliowazunguka, Yoshua alipokuwa amezeeka na umri wake kusonga sana,^b **2** Yoshua aliwaita Waisraeli wote,^c wazee wao, viongozi wao, waamuzi wao, na wakuu wao,^d akawaambia hivi: “Nimezeeka na umri wangu umesonga sana. **3** Ninyi wenyewe mmeona mambo yote ambayo Yehova Mungu wenu aliyatendea mataifa haya yote kwa ajili yenu, kwa sababu Yehova Mungu wenu ndiye aliyekuwa akiwapigania.^e **4** Tazameni, niliwagawia kwa kura^f nchi ya mataifa yanayobaki na pia nchi ya mataifa yote ambayo niliyaangamiza^g ili iwe urithi wa makabila yenu,^h kuanzia Yordani mpa-

22:34 *Maelezo haya yanaonyesha kwa-mba huenda madhabahu hiyo iliitwa Ushahidi au Ushuhuda.

ka Bahari Kuu* upande wa magharibi. **5** Na Yehova Mungu wenu ndiye aliyekuwa akiwafukuza kutoka mbele yenu,^a naye akawaondoa* kwa ajili yenu, nanyi mkamiliki nchi yao, kama Yehova Mungu wenu alivyowaahidi.^b

6 "Basi iweni jasiri sana mshike na kutekeleza mambo yote yaliyoandikwa katika kitabu cha Sheria^c ya Musa, msiiache kamwe na kwenenda kulia wala kushoto,^d

7 na msishirikiane kamwe na mataifa haya^e yaliyobaki kati yenu. Hampaswi hata kutaja majina ya miungu yao^f wala kuapa kwa majina hayo, na hampaswi kamwe kuiabudu au kuiinamia.^g **8** Bali mnapaswa kushikamana na Yehova Mungu wenu,^h kama vile ambavyo mmekuwa mkifanya mpaka sasa. **9** Yehova atafukuza mataifa makubwa na yeye nguvu kutoka mbele yenu,ⁱ kwa kuwa mpaka sasa hakuna mtu yeyote ambaye amewashinda ninyi.^j **10** Mtu mmoja tu kati yenu atawakimbiza watu elfu,^k kwa sababu Yehova Mungu wenu anawapigania,^l kama alivyowaahidi.^m **11** Basi jilindeni daima*ⁿ kwa kumpenda Yehova Mungu wenu.^o

12 "Lakini mkimwacha na kushikamana na watu wa mataifa haya yaliyobaki^p na kuoana nao^q na kushirikiana nao, **13** mjue kwa haki-ka kwamba Yehova Mungu wenu hataendelea kuyafukuza* mataifa haya kwa ajili yenu.^r Yatakuwa mtego wa ku-

23:4 *Yaani, Mediterania. **23:5** *Au "akachukua nchi yao." **23:11** *Au "lindeni nafsi zenu kwa uangalifu." **23:13** *Au "kuchukua nchi ya."

SURA YA 23

a Kut 23:30
Kut 33:2
Kum 11:23

b Hes 33:53

c Kut 24:7
Kum 17:18
Kum 31:26

d Kum 5:32
Kum 12:32
Yos 1:7, 8

e Kut 23:33
Kum 7:2

f Kut 23:13

g Kut 20:5

h Kum 10:20
Yos 22:5

i Kum 11:23

j Yos 1:3-5

k Law 26:8
Amu 3:31
2Sa 23:8

l Kut 23:27
Kum 3:22

m Kum 28:7

n Kum 4:9
Yos 22:5

o Kum 6:5

p Kut 23:29
Yos 13:2-6

q Kut 34:16
Kum 7:3
Amu 3:6
1Fa 11:4
Ezr 9:2

r Amu 2:3, 21

Safu ya 2

a Hes 33:55

b Yos 21:45
1Fa 8:56

c Law 26:3-12
Kum 28:1

d Law 26:14-17
Kum 28:15, 63

e 2Fa 24:20

f Yos 23:12, 13

SURA YA 24

g Kut 18:25
Yos 23:2

h Mwa 11:28, 31

i Mwa 11:26, 27

wanasa, nayo yatakuwa mjeledi wa kuwachapa mbavuni^a na miiba machoni mwenu mpaka mtakapoangamia kutoka katika nchi hii nzuri ambayo Yehova Mungu wenu amewapa.

14 "Basi sasa nakaribia kufa,* nanyi mnajua viziria kwa mioyo yenu yote na kwa nafsi[#] zenu zote kwamba halikukosa kutimia hata neno moja kati ya ahadi zote nzuri ambazo Yehova Mungu wenu aliwaahidi. Zote zimetimia kwenu. Halikukosa kutimia hata neno moja aliloahidi.^b **15** Lakini kama zilivyotimia ahadi zote nzuri alizowaahidi Yehova Mungu wenu,^c vivyo hivyo Yehova atawaletea misiba yote aliyoahidi* na kuwaangamiza kutoka katika nchi hii nzuri ambayo Yehova Mungu wenu amewapa.^d **16** Mkivunja agano la Yehova Mungu wenu alilowaamuru mshike na mkienda kuabudu miungu mingine na kuiinamia, hasira ya Yehova itawaka dhidi yenu^e nanyi mtaangamia haraka kutoka katika nchi nzuri ambayo amewapa."^f

24 Kisha Yoshua akayakua sanya makabila yote ya Israeli huko Shekemu, akawaita wazee wote wa Israeli, viongozi wao, waamuzi wao, na wakuu wao,^g nao wakasimama mbele za Mungu wa kweli. **2** Yoshua akawaambia watu wote, "Hivi ndivyo anavyosema Yehova Mungu wa Israeli, 'Zamani za kale^h mababu zenu,ⁱ kutia ndani Tera baba ya Abrahamu na baba ya Nahori, waliishi

23:14 *Tnn., "Leo ninafuata njia ya dunia yote." [#] Angalia Kamusi, uku. 2012. **23:15** *Au "mabaya yote."

ng'ambo ya Mto,* nao wali-kuwa wakiabudu miungu mi-ngine.^a

3 “Baada ya muda nili-
mtoa babu yenu Abraha-
mu^b ng'ambo ya Mto* na ku-
mtembeza katika nchi yote
ya Kanaani na kuzidisha
uzao wake.^c Nikampa Isaka;^d

4 naye Isaka nikampa Yakobo
na Esau.^e Baadaye nikampa
Esau Mlima Seiri ili aumiliki;^f
na Yakobo na wanawe waka-
shuka Misri.^g **5** Baadaye nili-
watuma Musa na Haruni,^h ni-
kaiileta Misri mapigo,ⁱ kisha
nikawatoa ninyi. **6** Nilipoku-
wa nikiwatoa mababu zenu
Misri,^j mlifika baharini, Wa-
misri waliwafuatia wakiwa na
magari ya vita na askari wapa-
nda farasi mpaka kwenye Ba-
hari Nyekundu.*^k **7** Na ma-
babu zenu wakaanza kumli-
lia Yehova,^l basi akaweka giza
kati yenu na Wamisri na kui-
leta bahari juu yao ikawafu-
nika Wamisri,^m na mliona kwa
macho yenu wenyewe mambo
niliyoyafanya huko Misri.ⁿ Ki-
sha mkaishi nyikani kwa mia-
ka mingi.*^o

8 “Nami nikawaleta katika
nchi ya Waamori waliokuwa
wakiishi ng'ambo ya* Yordani,
nao wakapigana nanyi.^p La-
kini niliwatia mikononi mwe-
nu ili mmiliki nchi yao, ni-
kawaangamiza kutoka mbele
yenu.^q **9** Kisha Balaki mwa-
na wa Sipori, mfalme wa Moa-
bu, akaja kupigana na Israeli.
Basi akamwita Balaamu mwa-
na wa Beori ili awalaani ni-
nyi.^r **10** Lakini sikumsikili-
za Balaamu.^s Basi akawaba-

24:2, 3, 14, 15 *Yaani, Mto Efrati. **24:3**
“Tnn., “mbegu yake.” **24:6** *Au “Baha-
ri ya Shamu.” **24:7** *Tnn., “siku nyingi.”
24:8 *Yaani, upande wa mashariki wa.

SURA YA 24

a Yos 24:15

b Mwa 12:1
Ne 9:7
Mdo 7:2

c Mwa 15:1, 5

d Mwa 21:3

e Mwa 25:26

f Mwa 36:8
Kum 2:5

g Mwa 46:2, 3

h Kut 3:10

i Kut 11:1

j Kut 12:37

k Kut 14:9

l Kut 14:10

m Kut 14:20, 27
Zb 106:11n Kut 3:20
Kum 4:34

o Hes 14:34

p Hes 11:23

q Ne 9:22

r Hes 22:2, 5
Kum 23:3, 4

s Hes 22:12

Safu ya 2

a Hes 23:11, 25
Hes 24:10

b Hes 31:7, 49

c Yos 3:17

d Yos 5:10

e Yos 11:16
Yos 21:44
Ebr 11:30f Kut 23:28
Yos 2:9, 10

g Zb 44:3

h Yos 11:14

i Kum 6:10, 11
Kum 8:7, 8j Mwa 17:1
Kum 10:12
Kum 18:13

k 1Sa 12:24

l Law 17:7
Eze 23:8m Kum 30:19, 20
1Fa 18:21

n Yos 24:2

o Kut 23:32
Kum 7:25
Amu 6:10

p Amu 10:6

riki ninyi tena na tena,^a nami
nikawaokoa kutoka mikononi
mwake.^b

11 “Kisha mkavuka Yorda-
ni^c na kufika Yeriko.^d Nao vi-
ngozi* wa Yeriko, Waamori,
Waperizi, Wakanaani, Wahiti,
Wagirgashi, Wahivi, na Waye-
busi wakapigana nanyi, lakini
nikawatia mikononi mwenu.^e

12 Basi nikawafanya wavunji-
ke moyo* kabla ya ninyi ku-
fika, nao wakakimbia^f—wafal-
me wawili wa Waamori. Ha-
mkuwashinda kwa sababu
ya upanga wenu wala upinde
wenu.^g **13** Kwa hiyo niliwa-
pa nchi ambayo hamkuipa-
ta kwa jasho lenu na majiji
ambayo hamkujenga,^h nanyi
mkakaa humo. Mnakula matu-
nda ya mizabibu na ya mizei-
tuni ambayo hamkupanda.ⁱ

14 “Kwa hiyo, mwoyopeni
Yehova na kumtumikia kwa
utimilifu[†] na uaminifu,[‡] on-
doeni miungu ambayo ma-
babu zenu waliabudu ng'ambo
ya Mto* na nchini Misri,^k
nanyi mtumikieni Yehova.

15 Sasa ikiwa mnaona ni vi-
baya kumtumikia Yehova, cha-
gueni leo yule mtakayemtum-
ikia,^l iwe ni miungu ambayo
mababu zenu waliabudu
ng'ambo ya Mto*^m au miungu
ya Waamori mnaoishi katika
nchi yao.ⁿ Lakini mimi na fa-
milia[†] yangu, tutamtumikia
Yehova.”

16 Ndipo watu wakajibu
hivi: “Hatuwezi kamwe kuwa-
zia kumwacha Yehova na
kuabudu miungu mingine.
17 Yehova Mungu wetu ndiye
aliyetuoa sisi na mababu zetu

24:11 *Au labda, “wamiliki wa masha-
mba.” **24:12** *Au labda, “waogope;
watishike.” **24:14** #Au “bila lawama.”
†Au “ukweli.” **24:15** #Au “nyumba.”

katika nchi ya Misri,^a katika nyumba ya utumwa,^b na kufanya miujiza mikubwa mbele ya macho yetu^c na kutulinda katika safari yetu yote na miongoni mwa watu wote ambao tulipita katikati yao.^d **18** Yehova aliyafukuza mataifa yote, kutia ndani Waamori, walioishi katika nchi hii kabla yetu. Kwa hiyo, sisi pia tutamtumikia Yehova, kwa sababu yeye ni Mungu wetu.”

19 Kisha Yoshua akawaambia watu, “Hamwezi kumtumikia Yehova, kwa maana yeye ni Mungu mtakatifu,^e ni Mungu anayetaka watu wamwabudu yeye peke yake.^f Hatawasamehe uasi wenu na dhambi zenu.^g **20** Mkinwachacha Yehova na kuabudu miungu ya kigeni, yeye pia atawaacha na kuwaangamiza hata ingawa amewatendea mema.”^h

21 Lakini watu wakamwambia hivi Yoshua: “Hapana, tutamtumikia Yehova!”ⁱ

22 Basi Yoshua akawaambia, “Ninyi ni mashahidi dhidi yenu wenyewe kwamba mmechagua kwa hiari yenu kumtumikia Yehova.”^j Nao wakajibu, “Sisi ni mashahidi.”

23 “Basi, ondoeni miungu ya kigeni iliyo kati yenu, mwelekeze mioyo yenu kwa Yehova Mungu wa Israeli.”
24 Watu wakamwambia Yoshua, “Tutamtumikia Yehova Mungu wetu, nasi tutaitii sauti yake!”

25 Kwa hiyo Yoshua akafanya agano na Waisraeli siku hiyo, akawapa maagizo na sheria huko Shekemu. **26** Kisha Yoshua akaandika maneno hayo katika kitabu

SURA YA 24

a Kut 19:4
Kum 32:12

b Kum 6:12

c Kut 14:31
Kum 4:34
Kum 29:2

d Kut 23:23

e Law 19:2
Zb 99:5
Isa 6:3
Ipe 1:15

f Kut 20:5
Kut 34:14
Hes 25:11
Mt 4:10

g Kut 23:20, 21
Hes 14:35

h Kum 28:15, 20
Yos 23:16
2Nya 15:2
Isa 63:10
Yer 17:13

i Kut 19:8

j Kum 26:17
Yos 24:15

Safu ya 2

a Kum 31:26

b Mwa 31:45

c Mwa 31:48

d Amu 2:6

e Amu 2:8, 9

f Yos 19:49, 50

g Kum 31:12, 13
Amu 2:7

h Mwa 50:25
Kut 13:19
Ebr 11:22

i Mwa 33:18, 19

j Mdo 7:15, 16

k Yos 20:7

l Hes 3:4
Hes 20:26

m Kut 6:25
Amu 20:28

cha Sheria^a ya Mungu, akachukua jiwe kubwa^b na kuliweka chini ya mti mkubwa kando ya mahali patakatifu pa Yehova.

27 Ndipo Yoshua akawaambia watu wote, “Tazameni! Jiwe hili litakuwa ushahidi dhidi yetu,^c kwa sababu lime sikia maneno yote ambayo Yehova ametuambia, nalo litakuwa ushahidi dhidi yenu, ili msimkane Mungu wenu.”

28 Basi Yoshua akawaruhusu watu waende zao, nao wakaenda kila mtu kwenye urithi wake.^d

29 Baada ya mambo hayo, Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Yehova, akafa akiwa na umri wa miaka 110.^e

30 Basi wakamzika kwenye eneo lake la urithi kule Timnath-sera,^f katika eneo lenye milima la Efraimu, upande wa kaskazini wa Mlima Gaashi. **31** Waisraeli waliondelea kumtumikia Yehova siku zote za Yoshua na siku zote za wazee walioendelea kuishi baada ya Yoshua kufa ambao walikuwa wameona mambo yote makuu ambayo Yehova aliwatendea Waisraeli.^g

32 Na mifupa ya Yosefu,^h ambayo Waisraeli walikuwa wameleta kutoka Misri, wakaizika huko Shekemu katika shamba ambalo Yakobo alinunua kwa vipande 100 vya fedhaⁱ kutoka kwa wana wa Hamori,^j baba ya Shekemu; nalo likawa urithi wa wana wa Yosefu.^k

33 Pia, Eleazari mwana wa Haruni akafa.^l Wakamzika katika Kilima cha Finehasi mwanawe,^m alichopewa katika eneo lenye milima la Efraimu.

WAAMUZI

YALIYOMO

- 1 Ushindi wa kabila la Yuda na la Simeoni (1-20)
Wayebusi waendelea kuishi Yerusalemu (21)
Yosefu achukua Betheli (22-26)
Wakanaani hawakufukuzwa wote (27-36)
- 2 Onyo kutoka kwa malaika wa Yehova (1-5)
Kifo cha Yohua (6-10)
Mungu atuma waamuzi kuwaokoa Waisraeli (11-23)
- 3 Yehova awajaribu Waisraeli (1-6)
Othnieli, mwamuzi wa kwanza (7-11)
Mwamuzi Ehudi amua Mfalme Egloni aliyekuwa mnene (12-30)
Mwamuzi Shamgari (31)
- 4 Mfalme Yabini wa Kanaani awakandamiza Waisraeli (1-3)
Nabii wa kike Debora na Mwamuzi Baraka (4-16)
Yaeli amua Sisera mkuu wa jeshi (17-24)
- 5 Wimbo wa ushindi wa Debora na Baraka (1-31)
Nyota zapigana na Sisera (20)
Mafuriko ya Mto Kishoni (21)
Wanaompenda Yehova wako kama jua (31)
- 6 Wamidiani wawakandamiza Waisraeli (1-10)
Malaika amhakikishia Mwamuzi Gideoni atapata msaada (11-24)
Gideoni abomoa madhabahu ya Baali (25-32)
Roho ya Mungu yamtia nguvu Gideoni (33-35)
Jaribio la manyoya (36-40)
- 7 Gideoni na wanaume 300 (1-8)
Jeshi la Gideoni lawashinda Wamidiani (9-25)
"Upanga wa Yehova na wa Gideoni!" (20)
Kambi ya Wamidiani yachanganyikiwa (21, 22)
- 8 Waefraimu wamlalamikia Gideoni (1-3)
Wafalme Wamidiani wafuatiliwa na kuuawa (4-21)
Gideoni akataa kuwa mfalme (22-27)
Historia fupi ya maisha ya Gideoni (28-35)
- 9 Abimeleki awa mfalme kule Shekemu (1-6)
Fumbo la Yothamu (7-21)
Utawala wa kikatili wa Abimeleki (22-33)
Abimeleki ashambulia Shekemu (34-49)
Mwanamke amjeruhi Abimeleki; Abimeleki afa (50-57)
- 10 Waamuzi Tola na Yairi (1-5)
Waisraeli waasi na kutubu (6-16)
Waamoni wataka kuwashambulia Waisraeli (17, 18)
- 11 Mwamuzi Yeftha afukuzwa, baadaye afanywa kuwa kiongozi (1-11)
Yeftha azungumza na Waamoni (12-28)
Nadhiri ya Yeftha na binti yake (29-40)
Maisha ya useja ya binti yake (38-40)
- 12 Apigana na Waefraimu (1-7)
Jaribio la kutamka Shibolet (6)
Waamuzi Ibzani, Eloni, na Abdoni (8-15)
- 13 Malaika amtembelea Manoa na mke wake (1-23)
Samsoni azaliwa (24, 25)
- 14 Mwamuzi Samsoni atafuta mke Mfilisti (1-4)
Roho ya Yehova yamwezesha Samsoni kumuua simba (5-9)
Samsoni atega kitendawili kwenye harusi (10-19)
Mwanamume mwingine apewa mke wa Samsoni (20)
- 15 Samsoni alipiza kisasi dhidi ya Wafilisti (1-20)
- 16 Samsoni akiwa Gaza (1-3)
Samsoni na Delila (4-22)
Samsoni alipiza kisasi na kufa (23-31)

- 17 Sanamu za Mika na kuhani wake (1-13)
 18 Watu wa kabila la Dani watafuta nchi (1-31)
 Kuchukuliwa kwa sanamu za Mika na kuhani wake (14-20)
 Jiji la Laishi lachukuliwa na kuitwa Dani (27-29)

- lbada ya sanamu katika jiji la Dani (30, 31)
 19 Wabenjamini wabaka katika jiji la Gibea (1-30)
 20 Wabenjamini washambuliwa (1-48)
 21 Kabila la Wabenjamini laokolewa (1-25)

1 Baada ya kifo cha Yohua,^a Waisraeli* walimuuliza Yehova,^b “Ni nani kati yetu atakayeenda kwanza kupigana na Wakanaani?” **2** Yehova akawajibu, “Kabila la Yuda litaenda kwanza kupigana nao.^c Tazama! Ninaitia nchi hiyo mikononi mwao.”* **3** Ndipo watu wa kabila la Yuda wakaambia ndugu zao wa kabila la Simeoni, “Twendeni pamoja katika eneo tulilopewa*^d tukapigane na Wakanaani. Nasi tutaenda nanyi katika eneo mlilopewa.” Basi watu wa kabila la Simeoni wakaenda pamoja nao.

4 Watu wa kabila la Yuda walipoenda, Yehova akawatia Wakanaani na Waperizi mikononi mwao,^e wakawashinda watu 10,000 huko Bezeki. **5** Wakamkuta Adoni-bezeki huko Bezeki, wakapigana naye na kuwashinda Wakanaani^f na Waperizi.^g **6** Adoni-bezeki akakimbia, wakamkimbiza na kumshika, wakamkata vidole gumba vya mikono na vya miguu. **7** Kisha Adoni-bezeki akasema, “Kuna wafalme 70 waliokatwa vidole gumba vya mikono na vya miguu wanaokota chakula chini ya meza yangu. Mungu ame-

1:1 *Tnn., “wana wa Israeli.” 1:2 *Au “Nimewapa nchi hiyo.” 1:3 *Tnn., “kura yangu.”

SURA YA 1

a Yos 24:29

b Hes 27:18, 21
Amu 20:18c Mwa 49:8
Kum 33:7
1Nya 5:2d Yos 15:1
Yos 19:1, 9

e Kum 9:3

f Mwa 10:6
Kum 20:17g Mwa 15:18-21
Kut 3:8
Amu 3:5
1Fa 9:20, 21

Safu ya 2

a Yos 15:8, 12

b Yos 15:63
Amu 1:21c Yos 11:16
Yos 15:20, 33d Yos 11:21
Yos 15:13, 14

e Yos 10:38

f Yos 15:15

g Hes 13:3, 6
Hes 14:24
Kum 1:35, 36
Yos 14:13

h Yos 15:16-19

i Amu 3:9

j 1Nya 4:13

nilipa kulingana na matendo yangu.” Baadaye wakampeleka Yerusalemu,^a akafia huko.

8 Kisha watu wa Yuda wakashambulia jiji la Yerusalemu^b na kuliteka; wakawau wakaaji wake kwa upanga na kuliteketeza jiji. **9** Baadaye watu wa Yuda wakaenda kupigana na Wakanaani waliokaa katika eneo lenye milima na waliokaa Negebu na Shefela.^c **10** Basi watu wa kabila la Yuda wakawashambulia Wakanaani waliokaa Hebroni (zamani Hebroni liliitwa Kiriatharba), nao wakamua She-shai, Ahimani, na Talmai.^d

11 Kisha wakawashambulia wakaaji wa Debiri.^e (Hapo awali Debiri liliitwa Kiriathseferi.)^f **12** Ndipo Kalebu^g akasema, “Yeyote atakayeshambulia na kuteka jiji la Kiriath-seferi, nitampa binti yangu Aksa awe mke wake.”^h **13** Othnieliⁱ mwana wa Kenasi,^j ndugu mdogo wa Kalebu, akaliteka. Kwa hiyo akampa Aksa binti yake awe mke wake. **14** Mwanamke huyo alipokuwa akienda nyumbani kwake, akamsihi mume wake amwombe baba* yake shamba. Kisha mwanamke huyo akashuka kutoka juu ya punda wake.[#]

1:14 *Yaani, baba ya Aksa. #Au labda, “akapiga makofi akiwa juu ya punda ili kumwita baba yake.”

Kalebu akamuuliza: “Unataka nini?” **15** Akamwambia, “Tafadhali nibariki, kwa maana umenipa shamba upande wa kusini,* nipe pia Gulothmaimu.”[#] Basi Kalebu akampa Gulothi ya Juu na Gulothi ya Chini.

16 Na wazao wa Mkeni,^a baba mkwe wa Musa,^b walitoka katika lile jiji la mite nde^c pamoja na watu wa Yuda na kwenda katika nyika ya Yuda, upande wa kusini wa Aradi.^d Wakakaa huko pamoja na wenyeji.^e **17** Lakini watu wa kabila la Yuda waka songa mbele pamoja na ndugu zao wa kabila la Simeoni, wakawashambulia Wakanaani waliokaa Sefathi na ku liangamiza jiji hilo.^f Kwa hiyo wakaliita Horma.^{*g} **18** Kisha watu wa kabila la Yuda waka teka Gaza^h na eneo lake, Ashkeloniⁱ na eneo lake, na Ekroni^j na eneo lake. **19** Yehova alikuwa pamoja na watu wa kabila la Yuda, nao wakamiliki eneo lenye milima, lakini hawakuweza kuwafukuza wakaaji wa bondeni,* kwa sababu walikuwa na magari ya vita yenye miundu ya chuma.^{#k} **20** Wakampa Kalebu jiji la Hebroni, kama Musa alivyoahidi,^l naye akawafukuza kutoka humo wale wana wata tu wa Anaki.^m

21 Lakini Wabenjamini hawakuwafukuza Wayebusi waliokaa Yerusalemu, kwa hiyo Wayebusi wanakaa na Wabenjamini jijini Yerusalemu mpaka leo.ⁿ

1:15 *Au “ eneo la Negebu.” [#]Yaani, “Chemchemi za (Mabakuli ya) Maji.” 1:17 *Maana yake “Maangamizi.” 1:19 *Au “nchi tamarare ya chini.” [#]Tnn., “magari ya chuma.”

SURA YA 1

a Hes 24:21
Amu 4:11

b Kut 3:1
Kut 4:18
Kut 18:1
Hes 10:29

c Kum 34:3
Amu 3:13

d Hes 21:1

e Hes 10:29-32

f Law 27:29
Kum 20:16

g Yos 19:1, 4

h Mwa 10:19
Yos 11:22

i Amu 14:19

j Yos 13:1-3
Yos 15:20, 45

k Kum 20:1
Yos 17:16

l Hes 14:24
Yos 14:9

m Hes 13:22

n Yos 15:63
2Sa 5:6

Safu ya 2

a Yos 14:4

b Mwa 49:22, 24
Yos 16:1
Zb 44:3

c Mwa 35:6

d Yos 6:25
1Sa 15:6

e Yos 21:8, 25
Amu 5:19

f Yos 17:11, 12

g Mwa 9:25
1Fa 9:20, 21

h Hes 33:55
Kum 7:2
Kum 20:16
Yos 17:13

i Yos 16:10
1Fa 9:16

j Yos 19:15, 16

k Kum 20:17
Amu 2:2

l Yos 11:8
Yos 19:28, 31

m Yos 19:29, 31

n Yos 19:30, 31

o Yos 21:8, 31

22 Wakati huo, watu wa nyumba ya Yosefu^a wakashambulia Betheli, na Yehova alikuwa pamoja nao.^b

23 Na nyumba ya Yosefu ikatuma watu wakapeleleze jiji la Betheli (zamani liliitwa Luzi),^c

24 na wapelelezi hao wakamwona mtu akitoka jijini. Wakamwambia, “Tafadhali tuonyeshe njia ya kuingia jijini, nasi tutakutendea kwa fadhili.”^{* 25} Basi akawaonyesha njia ya kuingia jijini, kisha wakawau watu wote kwa upanga, lakini wakamwacha huru mtu huyo na familia yake.^d

26 Naye akaenda katika nchi ya Wahiti, akajenga jiji na ku liita Luzi. Hilo ndilo jina la jiji hilo mpaka leo.

27 Watu wa kabila la Manase hawakumiliki Beth-sheani na miji yake,* Taanaki^e na miji yake, Dori na miji yake, Ibleamu na miji yake, na Megido na miji yake.^f Wakanaani hawakukubali kutoka katika nchi hiyo. **28** Waisraeli wali popata nguvu, waliwatumikisha Wakanaani,^g lakini hawakuwafukuza wote.^h

29 Wala Waefraimu hawakuwafukuza Wakanaani waliokaa Gezeri. Wakanaani waliendelea kukaa kati yao huko Gezeri.ⁱ

30 Watu wa kabila la Zabuloni hawakuwafukuza wakaaji wa Kitroni na wakaaji wa Nahaloli.^j Wakanaani waliendelea kukaa kati yao na kufanya kazi za kulazimishwa.^k

31 Waasheri hawakuwafukuza wakaaji wa Ako, Sidoni,^l Alabu, Akzibu,^m Helba, Afiki,ⁿ na Rehobu.^o **32** Basi Waasheri wakaendelea kukaa kati

1:24 *Tnn., “tutakuonyesha upendo mshikamanifu.” 1:27 *Au “miji jirani.”

ya Wakanaani waliokaa katika nchi hiyo, kwa sababu hawakuwafukuza.

33 Watu wa kabila la Naftali hawakuwafukuza wakaaji wa Beth-shemeshi na Beth-anathi,^a lakini waliendelea kuka kati ya Wakanaani.^b Wakawatumikisha wakaaji wa Beth-shemeshi na wa Beth-anathi.

34 Waamori waliwazuia watu wa kabila la Dani wasishuke bondeni,^{*} hivyo wakabaki milimani.^c **35** Kwa hiyo Waamori hawakukubali kutoa kwenye Mlima Heresi, na Aiyaloni,^d na Shaalbimu.^e Lakini watu wa nyumba ya Yosefu walipopata nguvu zaidi, waliwatumikisha. **36** Eneo la Waamori lilianza kwenye mwinuko wa Akrabimu,^f kuanzia Sela kwenda milimani.

2 Kisha malaika wa Yehova^g akatoka Gilgali^h na kwenenda Bokimu na kusema: "Niliwatoa Misri na kuwaleta katika nchi ambayo niliapa kwamba ningewapa mababu zenu.ⁱ Pia nikasema, 'Sitavunja kamwe agano langu pamoja nanyi.^j **2** Nanyi msifanye agano na wakaaji wa nchi hii,^k bomoeni madhabahu zao.'^l Lakini hamkutii sauti yangu.^m Kwa nini hamkutii? **3** Ndiyo maana nilisema, 'Sitawafukuza kutoka mbele yenu,ⁿ nao watakuwa mtego kwenu,^o nanyi mtashawishiwa kuifuata miungu yao.'^p

4 Malaika wa Yehova alipo waambia Waisraeli wote maneno hayo, watu wakaanza kulia kwa sauti kubwa. **5** Kwa hiyo wakapaita mahali hapo Bokimu,^{*} nao wakamtotea Yehova dhabihu hapo.

1:34 *Au "nchi tambarare ya chini."
2:5 *Maana yake "Wanaolia."

SURA YA 1

a Yos 19:38, 39
b Kum 7:2
c Yos 19:47
Amu 18:1
d Yos 10:12
e Yos 19:42, 48
f Hes 34:2, 4
Yos 15:3, 12

SURA YA 2

g Kut 23:20, 23
Yos 5:13, 14
h Yos 5:8, 9
i Mwa 12:7
Mwa 26:3
j Mwa 17:1, 7
Law 26:42
k Kut 23:32
Kum 7:2
2Ko 6:14
l Kut 34:13
Hes 33:52
m Amu 1:28
n Amu 2:20-23
o Hes 33:55
Yos 23:12, 13
p Kut 23:33
Kum 7:16
1Fa 11:2

Safu ya 2

a Yos 24:28
b Yos 23:3
Yos 24:31
c Yos 24:29
d Yos 19:49, 50
e Yos 24:30
f Amu 3:7
Amu 10:6
1Fa 18:17, 18
g Kum 31:16
h Kum 6:14
i Kut 20:5
j Amu 3:7
Amu 10:6
1Fa 11:5
k Amu 3:8
2Fa 17:20
Zb 106:40, 41
l Amu 4:2

6 Yoshua alipowaruhusu watu waende zao, kila Mwisraeli alienda kwenye eneo lake la urithi ili kuimiliki nchi.^a **7** Na watu wakaendelea kumtumikia Yehova sikuzote za Yoshua na sikuzote za wazee walioendelea kuishi baada ya Yoshua kufa ambao walikuwa wameona mambo yote makuu ambayo Yehova aliwatendea Waisraeli.^b **8** Kisha Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Yehova, akafa akiwa na umri wa miaka 110.^c **9** Basi wakamzika kwenye eneo lake la urithi kule Timnath-heresi^d katika eneo lenye milima la Efraimu, upande wa kaskazini wa Mlima Gaashi.^e **10** Na watu wote wa kizazi hicho wakafa na kuzikwa kama walivyozikwa mababu zao,^{*} na kizazi kingine kikatokea ambacho hakikumjua Yehova wala mambo aliyowafanyia Waisraeli.

11 Na Waisraeli wakatenda maovu machoni pa Yehova, wakaabudu* Mabaali.^f **12** Basi wakamwacha Yehova, Mungu wa baba zao, aliyewatoa katika nchi ya Misri.^g Nao wakafuata miungu mingine, miungu ya watu waliowazunguka,^h wakaiinamia, na hivyo wakamkasirisha Yehova.ⁱ **13** Wakamwacha Yehova na kuabudu Baali na sanamu za Ashtorethi.^j **14** Ndiipo hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Waisraeli, akawatia mikononi mwa wapora ji, nao wakapora mali zao.^k Akawatia* mikononi mwa maadui waliowazunguka^l wala

2:10 *Tnn., "wakakusanywa kwa mababu zao." Huu ni msemu wa kishairi unao-rejelea kifo. 2:11 *Au "wakatumikia."
2:14 *Tnn., "Akawauza."

hawakuweza tena kuwashinda maadui wao.^a **15** Popote walipoenda, mkono wa Yehova uliwapinga na kuwaletetea msiba,^b kama Yehova alivyokuwa amesema na kama Yehova alivyokuwa amewaapia,^c nao wakateseka sana.^d **16** Basi Yehova alikuwa akiwapa waamuzi ambao waliwaokoa kutoka mikononi mwa waporaji.^e

17 Lakini walikataa kuwakiliza hata waamuzi hao, nao walifanya ukahaba na miungu mingine na kuiinamia. Walicha haraka njia ambayo mababu zao walifuata, ambao waliitii amri za Yehova.^f Walikataa kutii. **18** Wakati wowote Yehova alipowapa waamuzi,^g Yehova alikuwa pamoja na mwamuzi huyo, akawaokoa kutoka mikononi mwa maadui wao sikuzote za mwamuzi huyo; kwa maana Yehova aliwahirumia^{*h} kwa sababu ya kilio chao cha uchungu kilichosababishwa na wale waliowakandamizaⁱ na wale waliowatesa.

19 Hata hivyo mwamuzi huyo alipokufa, walitenda tena mambo maovu zaidi kuliko baba zao kwa kuifuata miungu mingine, kuiabudu na kuiinamia.^j Hawakuacha mazoea yao na tabia yao ya ukaidi. **20** Mwishowe hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Waisraeli,^k akasema, "Kwa sababu taifa hili limevunja agano langu^l nililofanya na mababu zao, na halijanitii,^m **21** basi mimi sitafukuza kutoka mbele yao taifa hata moja ambalo Yoshua aliacha alipokufa.ⁿ **22** Nitafanya hivyo ili kuwajaribu Waisraeli nione kama wataishika njia yangu mimi,

2:18 *Au "alighairi."

SURA YA 2

a Law 26:17, 37
Kum 28:15, 25

b Kum 28:15

c Kum 4:25, 26

d Amu 10:9

e Amu 3:9
1Sa 12:11
Ne 9:27
Zb 106:43

f Amu 2:7

g Amu 3:9

h Kum 32:36
Zb 106:45

i Amu 4:3

j Amu 4:1
Amu 8:33

k Kum 7:4
Amu 10:7
Zb 106:40

l Kut 24:3, 8
Kut 34:27
Kum 29:1
Yos 13:16

m Law 26:14, 17

n Yos 13:1, 2

Safu ya 2

a Hes 33:55
Kum 8:2
Yos 23:12, 13
Amu 3:4

SURA YA 3

b Kum 8:2
Amu 2:10

c Amu 1:18, 19

d Yos 13:1, 4
Amu 1:31

e Yos 9:1, 2

f Yos 13:1, 6

g Hes 34:2, 8
Yos 13:1, 5

h Kut 23:33
Amu 2:21, 22

i Amu 1:29
Zb 106:34

j Kut 34:15, 16
Hes 25:1, 2
Kum 7:3, 4
1Fa 11:1, 4

k Kum 31:16
Amu 2:11
Amu 10:6

l Kut 34:13
Kum 12:3
Kum 16:21

Yehova,^a na kutembea katika njia hiyo kama baba zao walivyofanya." **23** Kwa hiyo Yehova akaruhusu mataifa hayo yabaki. Hakuyafukuza haraka, wala hakuyatia mikononi mwa Yoshua.

3 Haya ndiyo mataifa ambayo Yehova aliyaruhusu yabaki ili yawajaribu Waisraeli wote ambao hawakuwa wamepigana vita vyovyote katika nchi ya Kanaani^b

2 (kusudi vizazi vilivyofuata vya Waisraeli, yaani, wale ambao hawakuwa wameona vita wafunzwe vita): **3** watawala watano wa Wafilisti,^c Wakanaani wote, Wasidoni,^d na Wahivi^e waliokaa katika Mlima Lebanoni^f kutoka Mlima Baal-hermoni mpaka Lebo-hamathi.^{*g} **4** Nao walitumiwa kuwajaribu Waisraeli ili kuona kama watatii amri ambazo Yehova aliwapa baba zao kupitia Musa.^h **5** Kwa hiyo, Waisraeli waliishi miongoni mwa Wakanaani,ⁱ Wahiiti, Waamori, Waperizi, Wahiivi, na Wayebusi. **6** Waisraeli walioa mabinti kutoka mataifa hayo, na kuruhusu mabinti wao waolewe na wana wao, nao wakaanza kuabudu miungu yao.^j

7 Basi Waisraeli wakatenda maovu machoni pa Yehova, wakamsahau Yehova Mungu wao, na kuabudu Mabaali^k na miti mitakatifu.^{*l} **8** Ndiipo hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Waisraeli, naye akawatia^{*} mikononi mwa Kushan-rishathaimu mfalme wa Mesopotamia.[#] Na Waisraeli waka-

3:3 *Au "njia ya kuingia Hamathi." **3:7** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **3:8** *Tnn., "akawauza." #Tnn., "Aram-naharaimu."

mtumikia Kushan-rishathaimu kwa miaka minane. **9** Waisraeli walipomlilia Yehova awasaidie,^a Yehova aliwapa mwokozi ili awaokoe.^b Othniel^c mwana wa Kenasi, ndugu mdogo wa Kaleb. **10** Roho ya Yehova ikamjia,^d akawa wamuzi wa Israeli. Alipoenda vitani, Yehova alimtia Kushan-rishathaimu mfalme wa Mesopotamia* mikononi mwake, naye akamshinda Kushan-rishathaimu. **11** Baada ya hapo nchi ikawa na amani* kwa miaka 40. Kisha Othniel mwana wa Kenasi akafa.

12 Waisraeli wakaanza tena kutenda maovu machoni pa Yehova.^e Basi Yehova akamruhusu Egloni mfalme wa Moabu^f awashinde Waisraeli, kwa sababu walitenda maovu machoni pa Yehova. **13** Isitose Egloni akawakusanya Waamoni^g na Waamaleki.^h Nao wakawashambulia Waisraeli na kuliteka jiji la mitende.ⁱ **14** Na Waisraeli wakamtumikia Egloni mfalme wa Moabu kwa miaka 18.^j **15** Ndipo Waisraeli wakamlilia Yehova awasaidie.^k Basi Yehova akawapa mwokozi,^l Ehudi^m mwana wa Gera, Mbenjiminiⁿ aliyetumia mkono wa kushoto.^o Baada ya muda Waisraeli wakamtuma Ehudi apeleke ushuru kwa Egloni mfalme wa Moabu. **16** Ehudi akatenge neza upanga wenye makali pande mbili uliokuwa na urefu wa mkono mmoja,* akaufunga kiunoni ndani ya vazi lake upande wa kulia. **17** Kisha akampelekea Egloni mfalme

3:10 *Tnn., "Aramu." 3:11 *Tnn., "ikapumzika." 3:16 *Huenda ni mkono mfupi wenye urefu wa sentimita 38 hivi (inchi 15). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 3

a Kum 4:30

Amu 10:10, 15

b Amu 2:16, 18

Amu 3:15

c 1Nya 4:13

d Hes 11:16, 17

Amu 6:34

Amu 11:29

Amu 14:5, 6

Amu 15:14

1Sa 11:6

1Sa 16:13

2Nya 15:1

e Amu 2:19

f Mwa 19:36, 37

g Mwa 19:36, 38

Amu 11:4, 5

h Kut 17:8

Amu 6:3

i Kum 34:3

j Kum 28:48

k Zb 78:34

l Amu 3:9

m Amu 4:1

n Mwa 49:27

o Amu 20:15, 16

Safu ya 2

a Yos 4:19

Yos 5:8, 9

wa Moabu ushuru huo. Egloni alikuwa mnene sana.

18 Baada ya Ehudi kutoa ule ushuru, akaondoka pamoja na watu waliokuwa wameu-beba. **19** Lakini walipofika kwenye sanamu za mawe* huko Gilgali,^a akarudi kwa mfalme na kumwambia: "Nina ujumbe wako wa siri, Ee mfalme." Basi mfalme akasema, "Ondokeni!" Ndipo watumishi wake wote wakaondoka.

20 Naye Ehudi akamkaribia alipokuwa ameketi peke yake darini katika chumba chake chenye baridi. Kisha Ehudi akasema, "Nina ujumbe wako kutoka kwa Mungu." Kwa hiyo akasimama kutoka katika kiti chake cha ufalme. **21** Ndipo Ehudi akauchomoa upanga kwa mkono wake wa kushoto kutoka upande wa kulia wa kiuno chake na kumchoma mfalme tumboni. **22** Upanga ukazama tumboni mwake pamoja na mpini wake, na mafuta yakaufunika upanga huo kwa sababu hakuuchomoa, na kinyesi kikatoka.

23 Naye Ehudi akatoka nje kupitia barazani,* akafunga kwa ufunguo milango ya chumba cha darini. **24** Baada ya Ehudi kuondoka, watumishi wa mfalme walirudi na kuona milango ya chumba cha darini ikiwa imefungwa kwa ufunguo. Kwa hiyo wakasema, "Labda ameenda msalani katika chumba chake cha ndani." **25** Waliendelea kungoja kwa muda mrefu mpaka wakaabika, lakini walipoona kwamba hafungui milango ya chumba cha darini, wakachukua

3:19 *Au labda, "machimbo ya mawe."

3:23 *Au labda, "sehemu ya kuingizia hewa."

ufunguo na kuifungua, wakamwona bwana wao ameanuka sakafuni akiwa amekufa!

26 Ehudi akatoroka walipokuwa wanangoja, naye akapita karibu na sanamu za mawe,*^a akafika salama salimini kule Seira. **27** Alipofika huko, akapiga pembe*^b katika eno lenye milima la Efraimu;^c na Waisraeli wakushuka pamoja naye kutoka milimani, yeye akiwa mbele yao. **28** Ndipo akawaambia, "Nifuateni, kwa sababu Yehova amewatia maddui wenu, Wamoabu, mikononi mwenu." Nao wakamfuata, wakateka vivuko vya Yordani ili kuwazuia Wamoabu wasikimbie, na hawakumruhusu mtu yeyote avuke. **29** Wakati huo waliwaua Wamoabu wapatao 10,000,^d na wote walikuwa wanaume wenye nguvu na mashujaa; hakuna hata mmoja wao aliyeponyoka.^e **30** Basi siku hiyo Waisraeli wakawa-shinda Wamoabu; na nchi ikawa na amani* kwa miaka 80.^f

31 Baada ya Ehudi, akaja Shamgari^g mwana wa Anathi, aliyewaua wanaume 600 Wafilisti^h kwa mchokoo wa ng'ombe;ⁱ yeye pia aliwaokoa Waisraeli.

4 Baada ya Ehudi kufa, Waisraeli wakaanza tena kute-nda maovu machoni pa Yehova.^j **2** Kwa hiyo Yehova akawatia mikononi mwa* Yabini mfalme wa Kanaani,^k aliyetawala Hasori. Mkuu wa jeshi lake aliitwa Sisera, naye alishi Haroshethi^l ya mataifa.[#] **3** Waisraeli wakamlilia Yehova^m kwa sababu Yabini aliku-

3:26 *Au labda, "kwenye machimbo."
3:27 *Au "tarumbeta." 3:30 *Tnn., "ikapumzika." 4:2 *Tnn., "akawauza kwa." #Au "Harosheth-ha-goimu."

SURA YA 3

- a Amu 3:19
- b Amu 6:34
1Sa 13:3
- c Amu 7:24
- d Kum 28:7
- e Law 26:7,8
- f Amu 3:11
- g Amu 5:6
- h Yos 13:1, 2
- i Amu 15:3, 15
1Sa 17:47, 50

SURA YA 4

- j Amu 2:19
- k Amu 2:14
Amu 3:8
Amu 10:7
- l Amu 4:16
- m Amu 2:18
Amu 3:9
Zb 107:19

Safu ya 2

- a Yos 17:16
Amu 1:19
- b Kum 28:48
- c Kut 15:20
Zfa 22:14
Lu 2:36
Mdo 21:8, 9
- d Yos 18:21, 25
- e Mwa 28:17, 19
- f Ebr 11:32
- g Yos 21:32
- h 1Fa 18:40
Zb 83:9
- i Kum 20:1
- j Amu 4:21, 22
Amu 5:24, 26
- k Yos 20:7, 9
Yos 21:32
- l Amu 5:18

- m Hes 24:21
Amu 1:16
1Sa 15:6

wa na magari 900 ya vita yenye miundu ya chuma,*^a na kwa miaka 20 aliwakandamiza sana Waisraeli.^b

4 Basi Debora, nabii wa kike,^c mke wa Lapidothi, niye aliyekuwa mwamuzi wa Israeli wakati huo. **5** Naye alizoea kuketi chini ya mtende wa Debora uliokuwa kati ya Rama^d na Betheli^e katika eno lenye milima la Efraimu; Waisraeli walikuwa wakienda kwa-ke ili kupata maamuzi. **6** Akatuma mjumbe amwite Baraka^f mwana wa Abinoamu kutoka Kedesh-naftali,^g akamwambia, "Yehova Mungu wa Israeli anakuamuru hivi: 'Nenda* katika Mlima Tabori ukiwa na wanaume 10,000 kuto-ka kabila la Naftali na la Zabuloni. **7** Nitakuletea Sisera, mkuu wa jeshi la Yabini na magari yake ya vita na majeshi yake kwenye kijito cha* Kishoni,^h nami nitamtia mikononi mwako."ⁱ

8 Ndipo Baraka akamwambia, "Ukienda pamoja nami, nitaenda, lakini usipoenda pamoja nami, sitaenda." **9** Basi Debora akamwambia, "Hakika nitaenda pamoja nawe. Hata hivyo, hutapata sifa katika vita hivyo, kwa kuwa Yehova atamtia Sisera mikononi mwa mwanamke."^j Ndipo Debora akaenda pamoja na Baraka mpaka Kedeshi.^k **10** Baraka akawaita watu wa kabila la Zabuloni na Naftali^l waje Kedeshi, na wanaume 10,000 wakamfuata. Debora pia akamfuata.

11 Lakini Heberi Mkeni alikuwa amejitenga na Wakeni,^m

4:3 *Tnn., "magari 900 ya chuma." 4:6 *Au "Wapange wanaume wako kwa ajili ya vita." 4:7 *Au "korongo kavu la."

waliokuwa wazao wa Hobabu, baba mkwe wa Musa,^a naye alipiga hema lake karibu na mti mkubwa uliokuwa Saananimu, kule Kedeshi.

12 Wakamwambia Sisera kwamba Baraka mwana wa Abinoamu amepanda kwenenda kwenye Mlima Tabori.^b

13 Mara moja Sisera akakusanya magari yake yote ya vita—magari 900 yenye miundu ya chuma*—na wanajeshi wote walioandamana naye kutoka Haroshethi ya mataifa na kwenda kwenye kijito cha[#] Kishoni.^c **14** Ndipo Debora akamwambia Baraka: “Inuka! Kwa maana hii ndiyo siku ambayo Yehova atamtia Sisera mikononi mwako. Yehova anakutangulia.” Na Baraka akashuka Mlima Tabori akiifuatwa na wanaume 10,000.

15 Kisha Yehova akamvuruga^d Sisera na magari yake yote ya vita na jeshi lake lote na kuwaangamiza kwa upanga wa Baraka. Ndipo Sisera akatoka katika gari lake na kukimbia kwa miguu. **16** Baraka akayafuatia yale magari ya vita na lile jeshi mpaka Haroshethi ya mataifa. Jeshi lote la Sisera likaangamizwa kwa upanga; hakubaki hata mtu mmoja.^e

17 Lakini Sisera akakimbia kwa miguu mpaka kwenye hema la Yaeli^f mke wa Hebereri Mkeni,^g kwa maana kulikuwa na amani kati ya Yabini^h mfalme wa Hasori na nyumba ya Hebereri Mkeni. **18** Kisha Yaeli akatoka nje kumpokea Sisera, akamwambia, “Karibu bwana wangu, karibu ndani. Usiogope.” Basi akai-

4:13 *Tnn., “magari 900 ya chuma.”
#Au “korongo kavu la.”

SURA YA 4

a Hes 10:29

b Amu 4:6

c Amu 5:20, 21

d Kut 14:24
Yos 10:10

e Law 26:7

f Amu 5:24

g Amu 4:11

h Amu 4:1, 2

Safu ya 2

a Amu 5:25

b Amu 4:9
Amu 5:26, 27

c Ebr 11:32, 33

d Mwa 9:25

e Kum 7:24

SURA YA 5

f Amu 4:4

g Amu 4:6
Ebr 11:32h Kut 15:1
Zb 18:Uta

ngia ndani ya hema lake, naye Yaeli akamfunika kwa blanke-ti. **19** Sisera akamwambia, “Tafadhali, nipe maji kidogo ya kunywa, kwa maana nina kiu.” Basi Yaeli akafungua kiriba cha ngozi chenye maziwa na kumpa anywe,^a kisha akamfunika tena. **20** Sisera akamwambia, “Simama kwenye mlango wa hema, na mtu yeyote akija kukuuliza kama kuna yeyote hemani, mwambie, ‘Hakuna!’”

21 Lakini Yaeli mke wa Hebereri akachukua kigingi cha hema na nyundo. Kisha Sisera alipokuwa amelala usingizi mzito kwa sababu ya uchovu, Yaeli akaenda kimyakimya na kukipigilia kile kigingi kichwani mwake,^{*} nacho kikapenya mpaka udongoni, akafa.^b

22 Baraka alipokuwa anamtafuta Sisera, Yaeli akatoka nje kumpokea, akamwambia, “Njoo nikuonyeshe mtu unayemtafuta.” Baraka akamfuata hemani, akamwona Sisera akiwa amekufa, kigingi kikiwa kichwani mwake.

23 Basi siku hiyo, Mungu akamshinda Yabini mfalme wa Kanaani mbele ya Waisraeli.^c **24** Na Waisraeli wakaendelea kuwa na nguvu* na kumshinda Yabini mfalme wa Kanaani,^d mpaka walipomwangamiza Yabini mfalme wa Kanaani.^e

5 Siku hiyo Debora^f pamoja na Baraka^g mwana wa Abinoamu wakaimba wimbo huu:^h

2 “Kwa sababu ya nywele ndefu* katika Israeli,

4:21 *Yaani, pembeni mwa paji la uso kati ya jicho na sikio. 4:24 *Tnn., “mkono wa Waisraeli ukazidi kuwa na nguvu.” 5:2 *Au “mashujaa waliokuwa na nywele ndefu.”

Kwa sababu ya watu kuji-tolea,^a

Msifuni Yehova!

- 3** Sikilizeni, enyi wafalme!
Tegeni sikio, enyi wata-wala!

Nitamwambia Yehova.

Nitamwambia sifa* Yeho-va,^b Mungu wa Israeli.^c

- 4** Yehova, ulipotoka Seiri,^d
Ulipopiga mwendo kutoka eneo la Edomu,

Dunia ilitikisika, na mbi-ngu zikamwaga maji,
Naam, mawingu yakamwa-ga maji.

- 5** Milima iliyeyuka* mbele za uso wa Yehova,^e

Hata Sinai kutoka mbele za uso wa Yehova,^f Mu-ngu wa Israeli.^g

- 6** Katika siku za Shamgari^h
mwana wa Anathi,
Katika siku za Yaeli,ⁱ bara-bara hazikuwa na watu;
Wasafiri walipita vicho-choroni.

- 7** Wanavijiji katika Israeli walitoweka;
Walitoweka, mpaka mimi Debora^j nilipotokea,
Mpaka nilipotokea kama mama katika Israeli.^k

- 8** Walichagua miungu mipya;^l

Kisha kukawa na vita ma-langoni.^m

Hakuwa na ngao, wala mkuki,

Kati ya wanaume 40,000 katika Israeli.

- 9** Moyo wangu uko pamoja na makamanda wa Israeli,ⁿ

SURA YA 5

a Amu 4:10

b 2Sa 22:50
Zb 7:17

c Kut 20:2

d Kum 33:2

e Kum 4:11

f Kut 19:18
Ne 9:13

g Kut 20:2

h Amu 3:31

i Amu 4:17

j Amu 4:4

k Amu 4:5

l Kum 32:16, 17
Amu 2:12

m Amu 4:1-3

n Amu 4:6

Safu ya 2

a Amu 4:10

b Amu 4:4

c Amu 5:1

d Amu 4:6

e Hes 32:39

Waliojitolea na kwenda pamoja na watu.^a

Msifuni Yehova!

- 10** Ninyi mnaopanda juu ya punda wa hudhurungi,
Ninyi mnaoketi kwenye mazulia bora,
Nanyi mnaotembea bara-barani,
Fikirieni mambo haya!

- 11** Sauti za wanaoteka maji zilisikika mahali pa kute-ka maji;

Walisimulia matendo ya uadilifu ya Yehova,

Matendo ya uadilifu ya wa-navijiji katika Israeli.

Kisha watu wa Yehova wa-kashuka malangoni.

- 12** Amka, amka, Ee Debora!^b
Amka, amka, imba wimbo!^c

Inuka, Baraka!^d Wachukue mateka wako, Ee mwana wa Abinoamu!

- 13** Ndipo waliobaki wakashu-ka kwenda kwa watu ma-shuhuri;

Watu wa Yehova wakashu-ka kuja kwangu ili kupi-gana na wanaume wenye nguvu.

- 14** Walitoka Efraimu, wale walio bondeni;*
Wanakufuata, Ee Benjami-ni, kati ya watu wako.

Kutoka Makiri^e makama-nda walishuka,

Na kutoka Zabuloni wale wanaobeba fimbo za wa-naowaandikisha watu je-shini.[#]

- 15** Wakuu wa Isakari waliku-wa pamoja na Debora,

5:14 *Au "nchi tambarare ya chini."
#Au labda, "walio na vifaa vya mwa-ndishi."

5:3 *Au "Nitampigia muziki." 5:5 *Au labda, "ilitetemeka."

- Walikuwa pamoja naye kama Baraka^a alivyokuwa pamoja naye. Alipelekwa kwa miguu bondeni.*^b
- Kati ya vikundi vya Rubeni watu waliuchunguza sana moyo wao.
- 16** Kwa nini uliketi chini kama mnyama aliyelemelewa na mizigo,* Ukiwasikiliza wakiwapigia kondoo zumari?^c
- Kwa kuwa watu walisitaita sana kati ya vikundi vya Rubeni.
- 17** Watu wa Gileadi walibaki ng'ambo ya Yordani;^d Kabila la Dani, kwa nini mliendelea kukaa kwenye meli?^e
- Watu wa kabila la Asheri waliketi kizembe kando ya bahari, Na kuendelea kukaa bandarini.^f
- 18** Watu wa Zabuloni walihatarisha uhai wao* karibu wafe; Naftali pia,^g kwenye vilima vilivyo wazi.^h
- 19** Wafalme walikuja, wakapigana vita; Wafalme wa Kanaani wakapiganaⁱ
- Huko Taanaki, kando ya maji ya Megido.^j
- Hawakuchukua fedha kama nyara.^k
- 20** Kutoka mbinguni nyota zilipigana; Kutoka kwenye njia zake zilipigana na Sisera.

5:15 *Au "nchi tambarare ya chini."
5:16 *Au "Kwa nini uliketi kati ya mizigo miwili."
5:18 *Au "walidharau nafsi zao."

SURA YA 5

a Amu 4:6
Ebr 11:32

b Amu 4:14

c Hes 32:1

d Yos 22:9

e Yos 19:46, 48

f Yos 19:24, 29

g Amu 4:6, 10

h Amu 4:14

i Amu 4:13

j Amu 1:27

k Amu 4:16

Safu ya 2

a Amu 4:7, 13
Zb 83:9

b Zb 20:7
Met 21:31

c Amu 4:17

d Amu 4:11

e Amu 4:19

f Amu 4:21, 22

- 21** Mafuriko ya Kishoni yaliwafagilia* mbali.^a Mafuriko ya[#] kale, mafuriko ya[^] Kishoni. Uliwakanyaga wenye nguvu, Ee nafsi[®] yangu.
- 22** Ndipo kwato za farasi zilipokanyaga kwa kishindo Farasi dume walipokimbia kwa kasi.^b
- 23** 'Mlaani Merozi,' akasema malaika wa Yehova, 'Naam, walaani wakaaji wake, Kwa sababu hawakuja kumsaidia Yehova, Kumsaidia Yehova pamoja na mashujaa.'
- 24** Amebarikiwa sana Yaeli kati ya wanawake wote^c Mke wa Heberi^d Mkeni; Naam, amebarikiwa kuliko wanawake wote wanao-kaa katika mahema.
- 25** Aliomba maji; Yaeli aka-mpa maziwa. Alimpa maziwa ya mgando* katika bakuli kubwa.^e
- 26** Alinyoosha mkono wake akachukua kigingi cha hema, Na kwa mkono wake wa kulia akachukua nyundo ya fundi. Akampiga Sisera kwa nyundo, akamponda kichwa, Akampasua na kumtoboa kichwa.^f
- 27** Alianguka katikati ya miguu yake; alianguka na kulala kimya; Alianguka katikati ya miguu yake akafa;

5:21 *Au "Kijito cha Kishoni kiliwafagilia." #Au "Kijito cha." ^Au "kijito cha." ®Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:25 *Au "alimpa mtindi."

Alipoangukia, hapo ndipo alipolala akiwa ameshindwa.

- 28** Kupitia dirishani mwana-mke aliangalia nje, Mama ya Sisera alitazama kupitia viunzi vya dirisha,

'Mbona gari lake la vita limechelewa kuja?

Mbona vishindo vya kwato za farasi wake vimechelewa sana?'^a

- 29** Wanawake wenye hekima zaidi nyumbani mwake walimjibu;

Naam, yeye pia alisema tena na tena moyoni mwake,

- 30** 'Bila shaka wanagawana nyara walizopata, Msichana mmoja, wasichana wawili, kwa kila shujaa,

Nguo iliyotiwa rangi kwa ajili ya Sisera, nyara ya nguo iliyotiwa rangi,

Vazi lililopambwa,* nguo iliyotiwa rangi, mavazi mawili yaliyopambwa

Kwa ajili ya shingo za waliochukua nyara.'

- 31** Maadui wako wote na waangamie,^b Ee Yehova, Lakini wanaokupenda na wawe kama jua linalochomoza katika utukufu wake."

Na nchi ikawa na amani* kwa miaka 40.^c

- 6** Lakini Waisraeli wakatenda tena mambo maovu machoni pa Yehova,^d basi Yehova akawatia mikononi mwa Wamidiani kwa miaka saba.^e
2 Na Wamidiani wakawaka-

5:30 *Yaani, "vazi lililotariziwa." 5:31 *Tnn., "ikapumzika."

SURA YA 5

a Amu 4:15, 16

b Zb 83:9

c Amu 3:10, 11
Amu 3:30

SURA YA 6

d Amu 2:19

e Kum 28:15, 48
Amu 2:14
Ne 9:28

Safu ya 2

a Hes 33:55

b 1Sa 13:5, 6

c Amu 3:13

d Amu 8:10

e Kum 28:15, 33
Kum 28:31, 48

f Amu 8:10

g Amu 7:12

h Kum 4:30

i Amu 2:18
Zb 107:19

j Kut 20:2
Law 26:13
Amu 2:1

k Yos 10:42
Ne 9:24

l Kum 6:4

m Yos 24:15

n Kum 28:15
Amu 2:2
Yer 3:13

o Amu 2:1

p Yos 17:2
Amu 6:24
Amu 8:32

q Mwa 49:22, 24
Ebr 11:32

ndamiza Waisraeli.^a Kwa sababu ya Wamidiani, Waisraeli wakachimba mashimo ya kujificha* katika milima, mapango, na mahali pagumu kufikiwa.^b **3** Waisraeli walipopanda mbevu, Wamidiani, Waamaleki,^c na watu wa Mashariki^d waliwashambulia. **4** Nao walikuwa wakipiga kambi ili kuwashambulia na kuharibu mazao yote nchini hadi Gaza, na hawakuwaachia Waisraeli chakula chochote, wala kondoo, ng'ombe dume, au punda.^e **5** Walikuja na mifugo yao na mahema mengi sana kama nzige,^f na wao pamoja na ngamia wao hawangeweza kuhesabiwa,^g walikuja ili kuiharibu nchi. **6** Basi Wamidiani wakawafanya Waisraeli kuwa maskini sana; na Waisraeli wakamlilia Yehova awasaidie.^h

7 Waisraeli walipomlilia Yehova awasaidie kwa sababu ya Wamidiani,ⁱ **8** Yehova aliwaletea Waisraeli nabii aliye-waambia hivi: "Yehova Mungu wa Israeli anasema, 'Niliwatoa Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa.^j **9** Nikawao-koa kutoka mikononi mwa Wamisri na mikononi mwa wote waliowakandamiza, nikawafukuza mbele yenu na kuwapa ninyi nchi yao.^k **10** Kisha nikawaambia, "Mimi ni Yehova Mungu wenu.^l Msiogope miungu ya Waamori ambao mna-kaa katika nchi yao."^m Lakini hamkunitii."ⁿ

11 Baadaye malaika wa Yehova akaja^o na kuketi chini ya mti mkubwa wa Yoashi Mwabiezeri uliokuwa Ofra.^p Gideoni mwanawe^q alikuwa

6:2 *Au labda, "maghala yaliyo chini ya ardhii." 6:10 *Tnn., "hamkuisikiliza sauti yangu."

akipura ngano katika shinikizo la divai ili Wamidiani wasiione. **12** Ndipo malaika wa Yehova akamtokea, akamwambia hivi: “Yehova yuko pamoja nawe,^a ewe shujaa hodari.” **13** Gideoni akamwambia, “Niwie radhi, bwana wangu, lakini ikiwa Yehova yuko pamoja nasi, kwa nini mambo haya yote yametupata?^b Yako wapi matendo yake ya ajabu ambayo baba zetu walitusimulia,^c wakisema, ‘Yehova ndiye aliyettoa Misri?’^d Sasa Yehova ametuacha,^e naye ametutia mikononi mwa Wamidiani.” **14** Ndipo Yehova akamgeukia na kumwambia, “Nenda kwa nguvu ulizo nazo, nawe utawaokoa Waisraeli kutoka mikononi mwa Wamidiani.^f Je, si mimi ninayekutumama?” **15** Gideoni akamjibu, “Niwie radhi, Yehova. Ninawezaje kuwaokoa Waisraeli? Ukoo wangu ndio mdogo* zaidi katika kabila la Manase, nami ni mdogo kabisa katika nyumba ya baba yangu.” **16** Lakini Yehova akamwambia, “Kwa sababu nitakuwa pamoja nawe,^g utawashinda Wamidiani kana kwamba ni mtu mmoja.”

17 Ndipo Gideoni akamwambia, “Ikiwa nimepata kibali machoni pako, nionyeshe ishara kwamba ni wewe unayeongea nami. **18** Tafadhali usiondoke hapa mpaka nitakaporudi na kukuletea zawadi yangu na kuiweka mbele yako.”^h Basi akasema, “Sitandoka mpaka utakaporudi.” **19** Kwa hiyo Gideoni akaingia nyumbani na kutayarisha mwanambuzi na kuoka mikate isiyo na chachu kwa kutu-

6:15 *Tnn., “Elfu yangu ndiyo ndogo.”

SURA YA 6

a Amu 2:18

b Amu 6:2

c Kum 4:9
Zb 44:1

d Kut 13:14

e Kum 31:17
2Nya 15:2f Amu 8:22
Ebr 11:32g Kum 20:3, 4
Amu 2:18h Mwa 18:3, 5
Amu 13:15

Safu ya 2

a Mwa 18:6, 7
Mwa 19:1, 3b Law 9:24
Amu 13:19, 20
1Fa 18:38
1Nya 21:26
2Nya 7:1c Amu 13:8, 9
Ebr 13:2d Mwa 16:7, 13
Mwa 32:24, 30
Amu 13:21, 22
Lu 1:11, 12

e Da 10:19

f Mwa 22:14
Kut 17:15g Kut 23:24
Kum 12:3

mia efa* ya unga.^a Akaweka nyama katika kikapu na kutia mchuzi katika chungu cha kupikia; kisha akampelekea chini ya ule mti mkubwa.

20 Sasa yule malaika wa Mungu wa kweli akamwambia, “Chukua nyama na mikate hiyo isiyo na chachu, uviweke juu ya lile jiwe kubwa, na umimine mchuzi juu yake.” Akafanya hivyo. **21** Ndipo malaika wa Yehova akanyoosha fimbo iliyokuwa mkononi mwake na kwa ncha yake akaigusa ile nyama na ile mikate isiyo na chachu, na moto ukatoka kwenye lile jiwe na kuiteketeza ile nyama na ile mikate isiyo na chachu.^b Kisha malaika wa Yehova akatoweka. **22** Ndipo Gideoni akatambua kwamba huyo alikuwa malaika wa Yehova.^c

Mara moja Gideoni akasema, “Ole wangu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, kwa sababu nimemwona malaika wa Yehova uso kwa uso!”^d **23** Lakini Yehova akamwambia, “Uwe na amani. Usiogope;^e hutakufa.” **24** Basi Gideoni akamjengea Yehova madhabahu hapo, ambayo mpaka leo hii inaitwa Yehova-shalomu.^f Bado iko huko Ofra ya Waabiezeri.

25 Usiku huo Yehova akamwambia, “Mchukue ng’ombe dume mchanga wa baba yako, ng’ombe dume mchanga wa pili mwenye miaka saba, nawe ubomoe madhabahu ya Baali ambayo ni ya baba yako, na ukate mti mtakatifu* ulio kando yake.^g **26** Baada

6:19 *Efa ya unga ilikuwa karibu kilogramu 13. Angalia Nyongeza B14.
6:24 *Maana yake “Yehova Ni Amani.”
6:25 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

ya kumjengea Yehova Mungu wako madhabahu juu ya ngo-me hii kwa mawe yaliyopangwa vizuri, mchukue yule ng'ombe dume mchanga wa pili unitolee dhahabu ya kuteketewa juu ya kuni za ule mti mtakatifu* ambao ulikata." **27** Basi Gideoni akawachukua wanaume kumi kati ya watumishi wake na kufanya kama Yehova alivyomwambia. Lakini kwa kuwa aliwaogopa sana watu wa nyumba ya baba yake na wakaaji wa jiji, hakufanya mambo hayo mchana, aliyafanya usiku.

28 Wakaaji wa jiji wali-poamka asubuhi na mape-ma, waliona kwamba madhabahu ya Baali ilikuwa imebomolewa na ule mti mtakatifu* uliokuwa kando yake ulikuwa umekakwa, na yule ng'ombe dume mchanga wa pili alikuwa ameteketezwa juu ya madhabahu iliyokuwa imejengwa. **29** Wakaulizana, "Ni nani aliyefanya jambo hili?" Baada ya kufanya uchunguzi, wakasema, "Gideoni mwana wa Yoashi ndiye aliyefanya jambo hili." **30** Kwa hiyo wakaaji wa jiji wakamwambia hivi Yoashi: "Mtoe nje mwana wako, anapaswa kufa kwa sababu amebomoa madhabahu ya Baali na kukata mti mtakatifu* uliokuwa kando yake." **31** Ndipo Yoashi^a akawambia watu wote waliomkabili, "Je, ni lazima mumtete Baali? Je, ni lazima mumwokoe? Yeyote anayemtetea anapaswa kuuawa asubuhi hii.^b Ikiwa yeye ni mungu, acheni ajitete mwenyewe,^c kwa saba-

6:26, 28, 30 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 6

a Amu 6:11

b Kum 13:5
Kum 17:2-5c 1Fa 18:26, 27
Zb 115:5
Yer 10:5

Safu ya 2

a Hes 25:17, 18
Amu 6:2b Kut 17:16
Hes 24:20
Kum 25:19c Amu 6:3
Amu 7:12d Amu 3:9, 10
Amu 11:29
Amu 13:24, 25
Amu 14:6
Amu 15:14
Zek 4:6

e Amu 3:26, 27

f Yos 17:2

g Amu 6:14

bu mtu fulani amebomoa madhabahu yake." **32** Siku hiyo akamwita Gideoni jina Yerubaali,* akisema, "Acheni Baali ajitete mwenyewe, kwa sababu mtu fulani amebomoa madhabahu yake."

33 Wamidiani wote^a na Wamaleki^b na watu wa Mashariki wakaungana;^c wakavuka* na kupiga kambi katika Bonde la[#] Yezreeli. **34** Kisha roho ya Yehova ikamjia* Gideoni^d naye akapiga pembe,^{#e} na Waabiezeri^f wakakusanyika na kumfuata. **35** Akatuma wajumbe katika nchi yote ya kabila la Manase, wakakusanyika pia na kumfuata. Akatuma pia wajumbe kotekote katika nchi ya Asheri, Zabuloni, na Naftali, nao wakaja kutana naye.

36 Kisha Gideoni akamwambia hivi Mungu wa kweli: "Ikiwa utawaokoa Waisraeli kwa mkono wangu, kama ulivyoahidi,^g **37** ninaweka manyoya ya kondoo kwenye uwanja wa kupuria. Ikiwa kutakuwa na umande juu ya manyoya hayo peke yake lakini ardhi yote inayozunguka manyoya hayo iwe kavu, ndipo nitakapojua kwamba utawaokoa Waisraeli kwa mkono wangu, kama ulivyoahidi." **38** Na ikawa hivyo. Alipoamka mapema siku iliyofuata na kukamua manyoya hayo, maji ya umande yalijaa kwenye bakuli kubwa. **39** Hata hivyo, Gideoni akamwambia hivi Mungu wa kweli: "Tafadhali usinikasirikie, nakuo-

6:32 *Maana yake "Acheni Baali Ajitete Kisheria (Apambane)." 6:33 *Au "wakavuka mto." [#]Au "Nchi Tambarare ya Chini ya." 6:34 *Au "ikamfunika." [#]Au "tarumbeta."

mba jambo moja zaidi. Tafadhali niruhusu nifanye jaribio lingine moja tu kwa manyoya haya. Tafadhali, acha manyoya peke yake yawe makavu, na ardhi yote iwe na umande.”

40 Basi Mungu akafanya hivyo usiku huo; manyoya peke yake yakawa makavu, na ardhi yote ikawa na umande.

7 Ndipo Yerubaali, yaani, Gideoni,^a na watu wote waliokuwa pamoja naye wakaa mka mapema na kupiga kambi karibu na Chemchemi ya Harodi, nayo kambi ya Wamidiani ilikuwa bondeni* upande wa kaskazini wa kambi yao karibu na kilima cha More.

2 Yehova akamwambia Gideoni, “Watu ulio nao ni wengi sana kwangu mimi kuwatia Wamidiani mikononi mwao.^b Waisraeli wasije wakajigamba mbele zangu wakisema, ‘Mkono wangu mwenyewe ulinioko.’^c **3** Sasa tafadhali, watangazie hivi watu wote: ‘Mtu yeyote anayeogopa na kutetemeka, arudi nyumbani.’”^d Basi Gideoni akawajaribu kwa maneno hayo. Ndipo watu 22,000 wakarudi nyumbani, wakabaki watu 10,000.

4 Lakini Yehova akamwambia hivi Gideoni: “Watu hawa bado ni wengi sana. Wapeleke kwenye maji ili niwajaribu kwa ajili yako. Mtu yeyote nitakayekuambia, ‘Huyu ataenda pamoja nawe,’ ataenda pamoja nawe, lakini yeyote nitakayekwambia, ‘Huyu hataenda pamoja nawe,’ basi hataenda.” **5** Basi Gideoni akawa-peleka watu kwenye maji.

Kisha Yehova akamwambia Gideoni, “Watenganishe watu

SURA YA 7

a Amu 6:11, 32

b 1Sa 14:6
2Nya 14:11

c 1Sa 17:47

d Kum 20:8

Safu ya 2

a Amu 7:2

b Amu 6:33

c Amu 3:9,10
Amu 4:14

d Amu 6:33

wote wanaoramba maji kama mbwa anavyoramba na watu wanaopiga magoti kunywa maji.” **6** Wale waliochota maji kwa mikono yao na kuyaramba walikuwa wanauame 300. Lakini wengine wote walipiga magoti walipokunywa maji.

7 Sasa Yehova akamwambia hivi Gideoni: “Nitawatua wanaume hawa 300 walioramba maji kuwaokoa ninyi, nami nitawatia Wamidiani mikononi mwako.^a Lakini wambie wengine wote warudi nyumbani.” **8** Kwa hiyo wakachukua vyakula na pembe* za wanaume hao Waisraeli, kisha Gideoni akawaambia wote warudi nyumbani, akabaki na wale 300 peke yao. Kambi ya Wamidiani ilikuwa upande wa chini bondeni.^b

9 Usiku huo, Yehova akamwambia hivi: “Nenda uishambulie kambi, kwa maana nimeitia mikononi mwako.^c **10** Lakini ikiwa unaogopa kuishambulia, nenda kwanza kambini na Pura mtumishi wako. **11** Sikiliza wanayosema, nawe utapata ujasiri wa* kuwashambulia.” Ndipo yeye na Pura mtumishi wake wakashuka mpaka ukingoni mwa kambi hiyo ya kijeshi.

12 Wamidiani na Waamaleki na watu wote wa Mashariki^d walikuwa wamejaa bondeni nao walikuwa wengi kama nzige, na ngamia wao hawangeweza kuhesabiwa,^e walikuwa wengi kama chembe za mchanga kwenye ufuo wa bahari. **13** Gideoni alipofika, mtu fulani alikuwa

7:8 *Au “tarumbeta.” 7:11 *Tnn., “na mikono yako itakuwa na nguvu za.”

7:1 *Au “nchi tambarare ya chini.”

e Amu 6:3, 5

akimsimulia mwenzake ndoto, akisema, "Katika ndoto niliona mkate wa shayiri wa mvingo ukivingirika hadi kwenye kambi wa Wamidiani. Ukali-piga hema kwa nguvu na ku-liangusha.^a Naam, ukalipindua hema hilo, likaanguka chini."

14 Basi mwenzake akasema, "Bila shaka huo ni upanga wa Gideoni^b mwana wa Yoashi, mwanamume Mwisraeli. Mungu amewatia Wamidiani na kambi yote mikononi mwake."^c

15 Mara tu Gideoni alipomsikia akisimulia ndoto hiyo na kueleza maana yake,^d akainama chini na kuabudu. Kisha akarudi katika kambi ya Waisraeli na kusema, "Twendeni, kwa kuwa Yehova ameitia kambi ya Wamidiani mikononi mwenu." **16** Basi akawagawa wale wanaume 300 katika vikosi vitatu na kuwapa wote pembe^{*e} na mitungi mikubwa mitupu yenye mienne. **17** Akawaambia, "Nitazameni na kufanya kama tu nitakavyofanya. Nitakapofika kwenye ukingo wa kambi, fanyeni kama nitakavyofanya. **18** Nitakapopiga pembe,^{*} mimi na wote walio pamoja nami, ninyi pia zipigeni pembe^{*} kuizunguka kambi yote na kupaza sauti, 'Upanga wa Yehova na wa Gideoni!'"

19 Gideoni na wale wanaume 100 waliokuwa pamoja naye wakaja kwenye ukingo wa kambi mwanzoni mwa kesho la katikati ya usiku,^f baada tu ya askari walizinzi kuanza zamu. Wakazipiga zile pembe^{*f} na kuivunjavunja ile mi-

SURA YA 7

a Amu 6:16

b Amu 6:14

c Amu 7:7

d Amu 7:11

e Amu 7:8

f Amu 7:8

Safu ya 2

a Amu 7:16

b Kut 14:25
2Fa 7:6, 7

c 2Nya 20:23

d 1Fa 19:16

e Amu 6:35

f Zb 83:11
Isa 10:26

g Amu 8:4

tungi mikubwa waliyokuwa wamebeba mikononi mwao.^a

20 Ndipo vile vikosi vitatu vikapiga pembe^{*} na kuivunjavunja ile mitungi mikubwa. Wakashika mienne kwa mikonono ya kushoto na zile pembe kwa mikono ya kulia na kuzipiga, wakipaza sauti, "Upanga wa Yehova na wa Gideoni!" **21** Wakasimama kila mtu mahali pake kuizunguka ile kambi, na jeshi lote likakimbia huku likipiga kelele.^b **22** Wanaume hao 300 wakaelelea kupiga pembe,^{*} na Yehova akawafanya waanze kuuana wao kwa wao katika kambi yote;^c na jeshi likakimbia hadi Beth-shita, likafika Serera, hadi mpakani mwa Abel-mehola^d karibu na Tabathi.

23 Wanaume Waisraeli wakakusanywa kutoka katika kabila la Naftali, Asheri, na kabila lote la Manase,^e nao wakawafuatia Wamidiani. **24** Gideoni akatuma wajumbe katika eneo lote lenye milima la Efraimu, akisema, "Shukeni mkawashambulie Wamidiani, wazuieni wasivuke vijito vyote vya maji kufikia Beth-bara na pia Yordani." Basi watu wote wa Efraimu wakakusanyika pamoja, nao wakawazuia kuvuka vijito vyote vya maji kufikia Beth-bara na Yordani. **25** Pia wakawakamata wale wakuu wawili wa Midiani, yaani, Orebu na Zeebu; wakamuua Orebu juu ya mwamba wa Orebu^f na kumuua Zeebu kwenye shinikizo la divai la Zeebu. Wakaendelea kuwafuatia Wamidiani,^g nao wakamletea Gideoni kichwa cha Orebu na cha Zeebu katika eneo la Yordani.

7:16, 18-20, 22 *Au "tarumbeta." 7:19

^aKuanzia saa 4 hivi usiku hadi saa 8 usiku.

8 Ndipo watu wa Efraimu wakamuuliza Gideoni, “Kwa nini umetutendea hivi? Kwa nini hukutuita ulipoenda kupigana na Wamidiani?”^a Nao wakamshutumia vikali.^b

2 Lakini akawaambia, “Mimi nimefanya nini nikilinganishwa nanyi? Je, masalio ya Efraimu^c si bora kuliko mavuno ya zabibu ya Abiezeri?”^d

3 Mungu aliwatia mikononi mwenu Orebu na Zeebu,^e wakuu wa Midiani, lakini mimi nimefanya nini nikilinganishwa nanyi?” Gideoni aliposema hivyo* hasira yao ikapoa.[#]

4 Gideoni na wale wanaume 300 waliokuwa pamoja naye wakafika Yordani na kuvuka. Ingawa walikuwa wamechoka, waliendelea kuwafuatia maadui wao.

5 Akawaambia watu wa Sukothi, “Tafadhali wapeni mikate watu walio pamoja nami, kwa kuwa wamechoka nami ninawafuatia Zeba na Zalmuna, wafalme wa Midiani.”

6 Lakini wakuu wa Sukothi wakamwambia, “Je, tayari umewakamata Zeba na Zalmuna ili tuwape wanajeshi wako mikate?”

7 Ndipo Gideoni akawaambia, “Ni sawa, lakini Yehova atakapowatia Zeba na Zalmuna mikononi mwangu, nitawacharaza ninyi kwa miiba na michongoma ya nyikani.”^f

8 Naye akatoka huko na kwenda Penueli, akawaomba pia mikate, lakini watu wa Penueli wakamjibu kama watu wa Sukothi walivyomjibu.

9 Basi akawaambia pia watu wa Penueli, “Nitakaporudi baada ya kushinda, nitaubomoa mnara huu.”^g

8:3 *Tnn., “neno hilo.” #Tnn., “roho yao ikatulia.”

SURA YA 8

a Amu 7:2

b Amu 12:1
2Nya 25:10

c Amu 7:24

d Amu 6:11, 34

e Amu 7:24, 25

f Amu 8:16

g Amu 8:17

Safu ya 2

a Amu 7:12

b Hes 32:34, 35

c Amu 8:5, 6

d Amu 8:7

e Amu 8:8, 9

10 Basi Zeba na Zalmuna walikuwa Karkori pamoja na wanajeshi wao wapatao 15,000. Hao tu ndio waliobaki wa jeshi lote la watu wa Mashariki,^a kwa kuwa wenzao 120,000 waliotumia upanga waliuawa.

11 Gideoni akaeendelea kupanda kupitia eneo la watu waliokaa mahemani upande wa mashariki wa Noba na Yogbeha^b na kushambulia kambi ya maadui ambao hawakuwa wamejitayarisha kupigana.

12 Zeba na Zalmuna walipokimbia, Gideoni aliwafuatia na kuwakamata hao wafalme wawili wa Midiani, Zeba na Zalmuna, na jeshi lao lote likaogopa.

13 Kisha Gideoni mwana wa Yoashi akarudi kutoka vitani kupitia njia inayopanda kwenda Heresi.

14 Alipokuwa njiani, alimkamata kijana mmoja wa Sukothi na kumuuliza maswali. Basi kijana huyo akamwandikia majina 77 ya wakuu na wazee wa Sukothi.

15 Ndipo akarudi kwa watu wa Sukothi na kuwaambia, “Ndio hawa Zeba na Zalmuna ambao mlinidhiki kuwahusu mkisema, ‘Je, tayari umewakamata Zeba na Zalmuna ndipo tuwape mikate wanaume wako waliochoka?’”^c

16 Ndipo akawachukua wazee wa jiji hilo na kuwacharaza kwa miiba na michongoma ya nyikani, akawafunza somo wanaume wa Sukothi.^d

17 Kisha akabomoa mnara wa Penueli^e na kuwaua watu wa jiji hilo.

18 Akawauliza Zeba na Zalmuna, “Watu mliowaua kule Tabori walikuwaje?” Wakasema, “Walikuwa kama wewe, walikuwa kama wana wa

mfalme.” **19** Ndipo akasema, “Ni ndugu zangu, wana wa mama yangu. Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, ikiwa hamngewaua, mimi pia singewaua ninyi.” **20** Kisha akamwambia Yetheri mzaliwa wake wa kwanza, “Haya, waue.” Lakini kijana huyo hakuchomoa upanga wake; alio-gopa kwa sababu alikuwa kijana tu. **21** Basi Zeba na Zalmuna wakamwambia, “Tuue wewe mwenyewe, kwa maana mwanamume hujulikana kwa nguvu zake.”* Basi Gideoni akawaua Zeba na Zalmuna^a na kuchukua mapambo yenye umbo la mwezi mwandamo yaliyokuwa shingoni mwa ngamia wao.

22 Baadaye Waisraeli wakamwambia Gideoni, “Tutawale, wewe na mwana wako na mjukuu wako pia, kwa maana umetuokoa kutoka mikononi mwa Wamidiani.”^b **23** Lakini Gideoni akawaambia, “Mimi sitawatawala, wala mwanaangu. Yehova ndiye atakayewatawala.”^c **24** Pia akawaambia, “Ningependa kuomba jambo moja: Kila mmoja wenu anipe pete ya puani aliyochukua nyara.” (Walikuwa na pete za puani za dhahabu kwa sababu walikuwa Waishmaeli.)^d **25** Wakasema, “Tutakupa.” Basi wakatandaza nguo na kila mmoja wao akaweka pete ya puani aliyochukua nyara. **26** Na zile pete za puani za dhahabu ambazo aliwaomba zilikuwa na uzito wa shekeli 1,700 za dhahabu,* mbali na yale mapambo yenye umbo

8:21 *Tnn., “kwa maana jinsi mwanamume alivyo, ndivyo zilivyo nguvu zake.” **8:26** *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 8

a Zb 83:11

b Amu 6:14

c Kut 15:18
1Sa 10:19
Isa 33:22
Isa 43:15d Mwa 16:11
Mwa 25:13
Mwa 28:9
Mwa 37:28

Safu ya 2

a Amu 8:21

b Kut 28:6
Amu 17:5

c Amu 6:11

d Amu 2:17

e Zb 106:36

f Amu 6:1

g Amu 3:11
Amu 5:31h Amu 6:32
1Sa 12:11i Amu 9:1,2
2Sa 11:21

j Amu 6:11,24

k Amu 2:17,19
Amu 10:6

l Amu 9:4

m Amu 3:7

la mwezi mwandamo, hereni, mavazi ya sufu ya rangi ya zambarau yaliyovaliwa na wafalme Wamidiani, na mikufu iliyokuwa shingoni mwa ngamia.^a

27 Basi Gideoni akatumia dhahabu hiyo kutengeneza efodi*^b na kuiweka hadharani katika jiji lake la Ofra;^c na huko Waisraeli wote waka-fanya nayo ukahaba wa kiroho,^d ikawa mtego kwa Gideoni na kwa nyumba yake.^e

28 Hivyo Wamidiani^f wakashindwa na Waisraeli, na hawakupigana nao* tena; na nchi ikawa na amani^g kwa miaka 40 katika siku za Gideoni.^g

29 Basi Yerubaali^h mwana wa Yoashi akarudi nyumbani kwake na kukaa huko.

30 Gideoni akawa na wana 70,* kwa sababu alikuwa na wake wengi. **31** Na suria* wake aliyekuwa Shekemu akamzalia mwana, na Gideoni akamwita Abimeleki.ⁱ **32** Gideoni mwana wa Yoashi akafa baada ya kuishi maisha marefu, akazikwa katika kaburi la Yoashi baba yake katika jiji la Ofra la Waabiezeri.^j

33 Mara tu baada ya Gideoni kufa, Waisraeli wakaanza tena kufanya ukahaba wa kiroho na Mabaali,^k nao wakamfanya Baal-berithi kuwa mungu wao.^l **34** Na Waisraeli hawakumkumbuka Yehova Mungu wao^m aliyewao-koa kutoka mikononi mwa

8:27 *Au “kizibao cha kuhani.” **8:28** *Tnn., “hawakuinua kichwa chao.” **8:30** *Tnn., “alikuwa na wana 70 waliotoka katika viuno vyake.” **8:31** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

maadui wao waliowazunguka;^a **35** wala hawakuwa na upendo mshikamanifu kwa nyumba ya Yerubaali, yaani, Gideoni, aliyewatendea Waisraeli mambo mengi mema.^b

9 Baada ya muda Abimeleki mwana wa Yerubaali akaenda Shekemu kwa ndugu za mama yake na kwa familia yote ya babu yake,* akawaambia hivi: **2** "Tafadhali waulizeni viongozi wote* wa Shekemu, 'Je, ni afadhali zaidi kwenu kutawaliwa na wana wote 70 wa Yerubaali^d au na mtu mmoja tu? Kumbukeni kwamba mimi ni mfupa wenu na nyama yenu.'"#

3 Basi ndugu za mama yake wakawaambia viongozi wote wa Shekemu maneno hayo kwa niaba yake, nao wakamua kumfuata* Abimeleki kwa maana walisema: "Yeye ni ndugu yetu." **4** Wakampa Abimeleki vipande 70 vya fedha kutoka katika nyumba ya* Baal-berithi,^e naye akavitumia kuwakodi watu wanaozurura-zurura na wahuni ili wamfuate. **5** Kisha akaenda nyumbani kwa baba yake huko Ofra^f na kuwaua ndugu zake,^g wana 70 wa Yerubaali, juu ya jiwe moja. Yothamu mwana mdogo zaidi wa Yerubaali ndiye aliyeokoka peke yake, kwa sababu alijificha.

6 Kisha viongozi wote wa Shekemu na wakaaji wote wa Beth-milo wakakusanyika pamoja na kumweka Abimeleki

9:1 *Tnn., "familia ya nyumba ya baba ya mama yake." 9:2 *Au labda, "wamiliki wote wa mashamba." #Tnn., "nina uhusiano wa damu nanyi." 9:3 *Tnn., "mioyo yao ilielekea kumfuata." 9:4 *Au "hekalu la."

SURA YA 8

a Zb 106:43

b Amu 9:16-18

SURA YA 9

c Amu 8:30, 31

d Amu 8:30

e Amu 8:33
Amu 9:46

f Amu 6:11
Amu 8:27

g 2Fa 11:1
2Nya 21:4

Safu ya 2

a Kum 17:14
1Sa 8:7

b Kum 11:29
Yos 8:33
Yoh 4:20

c Amu 8:22

d Amu 9:6

e Amu 9:6

kuwa mfalme,^a karibu na ule mti mkubwa, penye nguzo iliyokuwa Shekemu.

7 Walipomwambia Yothamu habari hizo, akaenda mara moja na kusimama juu ya kilele cha Mlima Gerizimu,^b aka- waambia hivi kwa sauti kubwa: "Nisikilizeni, enyi viongozi wa Shekemu, naye Mungu atawasikiliza.

8 "Siku moja miti ilitaka kumtia mafuta mmoja wao awe mfalme. Basi ikauambia mzeituni, 'Tutawale.'^c **9** Lakini mzeituni ukaiambia, 'Je, niache kuzalisha mafuta yangu yanayotumiwa kumtukuzwa Mungu na wanadamu, niende kuitawala miti mingine?'

10 Kisha miti ikauambia mtini, 'Njoo ututawale.' **11** Lakini mtini ukaiambia, 'Je, niache kuzalisha matunda yangu matamu niende kuitawala miti mingine?' **12** Kisha miti ikauambia mzabibu, 'Njoo ututawale.' **13** Mzabibu ukasema, 'Je, niache kutoa divai yangu nzuri inayomfurahisha Mungu na wanadamu niende kuitawala miti?'

14 Mwishowe miti mingine yote ikauambia mkwamba,* 'Njoo ututawale.'^d **15** Ndipo mkwamba ukaiambia miti hiyo, 'Ikiwa kweli mnanitia mafuta niwe mfalme wenu, njooni mkae chini ya kivuli changu. Kama sivyo, moto na utoke ndani yangu na kuiteketeza mιεrezi ya Lebanoni.'

16 "Je, mmetenda kwa unyoofu na heshima kwa kumweka Abimeleki kuwa mfalme,^e na je, mmetenda wema Yerubaali na nyumba yake, je, mmetenda anavyostahili?

9:14 *Mkwamba ni mti wenye miiba.

17 Baba yangu alipowapigania,^a alihatarisha uhai wake* ili kuwaokoa kutoka mikoni ni mwa Wamidiani.^b **18** Lakin leo mmeasi nyumba ya baba yangu na kuwaua wanawe 70 juu ya jiwe moja.^c Kisha mkamweka Abimeleki, mwana wa kijakazi wake,^d awe mfalme juu ya viongozi wa Shekemu kwa sababu tu yeye ni ndugu yenu. **19** Basi ikiwa leo mmentendea Yerubaali na nyumba yake kwa unyoofu na heshima, shangilieni pamoja na Abimeleki naye pia ashangilie pamoja nanyi. **20** Kama sivyo, moto na utoke kwa Abimeleki na kuwateketeza viongozi wa Shekemu na Beth-milo,^e pia moto utoke kwa viongozi wa Shekemu na Beth-milo na kumtekeza Abimeleki.”^f

21 Ndipo Yothamu^g akakimbilia Beeru, akaishi huko kwa sababu alimwogopa Abimeleki ndugu yake.

22 Abimeleki alitawala* Israeli kwa miaka mitatu. **23** Ndipo Mungu akaacha uadui utokee* kati ya Abimeleki na viongozi wa Shekemu, nao wakamtendea Abimeleki kwa hila. **24** Hayo yalitokea ili kulipiza ukatili waliotendewa wale wana 70 wa Yerubaali, na ili hatia ya damu iwe juu ya Abimeleki ndugu yao kwa sababu aliwaua,^h na juu ya viongozi wa Shekemu kwa sababu walimsaidia kuuu ndugu zake. **25** Basi viongozi wa Shekemu wakaweka watu wamvizie Abimeleki milimani, wakamwibia kila mtu aliyepita karibu nao. Abimeleki akaambiwa mambo hayo.

9:17 *Au “nafsi yake.” 9:22 *Au “alijitwalia mamlaka juu ya.” 9:23 *Tnn., “akatuma roho mbaya.”

SURA YA 9

a Amu 7:9

b Amu 8:28

c Amu 9:5

d Amu 8:30, 31

e Amu 9:6, 49

f Amu 9:39, 53

g Amu 9:5

h Mwa 9:6
Amu 9:5

Safu ya 2

a Yos 21:20, 21
Yos 24:1

b Amu 8:33

c Amu 6:32

26 Basi Gaali mwana wa Ebedi na ndugu zake wakavuka kuingia Shekemu,^a nao viongozi wa Shekemu wakamtu-maini. **27** Wakaenda kuvuna zabibu katika mashamba yao ya mizabibu na kuzikanyaga katika shinikizo la divai, wakafanya sherehe, kisha wakaingia katika nyumba ya mungu wao,^b wakala, wakanywa, na kumlaani Abimeleki. **28** Ndipo Gaali mwana wa Ebedi akasema, “Abimeleki ni nani, na Shekemu ni nani ili tumtumikie? Je, yeye si mwana wa Yerubaali,^c na je, Zebuli si mjumbe wake? Watumikieni wana wa Hamori, baba ya Shekemu! Kwa nini tumtumikie Abimeleki? **29** Laiti watu hawa wangekuwa chini ya amri yangu, ningemwondoa Abimeleki.” Kisha akamwambia hivi Abimeleki: “Ongeza jeshi lako, uje tupigane.”

30 Zebuli mkuu wa jiji aliposikia maneno ya Gaali mwana wa Ebedi, akakasirika sana. **31** Kwa hiyo akawatuma kwa siri* wajumbe kwa Abimeleki, akisema, “Gaali mwana wa Ebedi na ndugu zake wako Shekemu, wanalichochea jiji likupinge. **32** Basi njoo usiku pamoja na watu wako mwavizie shambani. **33** Mara tu jua linapochomoza asubuhi, amkeni mapema mlishambulie jiji; atakapokuja na watu wake kuwashambulia, jitahidini kabisa kumshinda.”*

34 Basi Abimeleki na watu wake wote wakaja usiku, wakalivizia jiji la Shekemu wakiva vikosi vinne. **35** Gaali mwana wa Ebedi alipotoka nje na kusimama kwe-

9:31 *Au “hila.” 9:33 *Au “mtendeeni kadiri ya uwezo wenu.”

nye lango la jiji, Abimeleki na watu wake wakatoka mafichoni. **36** Gaali alipowaona, akamwambia Zebuli, "Tazama! Kuna watu wanaoshuka kutoka milimani." Lakini Zebuli akamwambia, "Unaona vivuli vya milima ukifikiri ni watu."

37 Baadaye Gaali akasema, "Tazama! Watu wanashuka kutoka katikati ya nchi, na kikosi kimoja kinakuja kupitia njia ya mti mkubwa wa Meonenimu." **38** Ndipo Zebuli akamwambia, "Umesahau ulivyojigamba ukisema, 'Abimeleki ni nani ili tumtumikie?'"^a Je, hawa si wale watu uliowadharau? Sasa nenda upigane nao."

39 Basi Gaali akawaongoza viongozi wa Shekemu kupigana na Abimeleki. **40** Gaali akashindwa na kukimbia, naye Abimeleki akamkimbiza, na watu wengi wakauawa mpaka kwenye lango la jiji.

41 Abimeleki akaendelea kukaa Aruma, naye Zebuli^b akawafukuza Gaali na ndugu zake kutoka Shekemu. **42** Kesho yake watu wakatoka na kwenda shambani, na Abimeleki akaambiwa jambo hilo. **43** Basi akachukua watu wake na kuwagawa katika vikosi vitatu na kuvizia shambani. Alipoona watu wakitoka jijini, akawashambulia na kuwaua. **44** Abimeleki na kikosi chake wakaenda mbio na kusimama kwenye lango la jiji, na vikosi viwili vikawashambulia na kuwaua watu wote waliokuwa shambani. **45** Abimeleki akapigana na jiji hilo siku nzima na kuliteka. Akawaua wakaaji wake, kisha akalibomoa jiji hilo^c na kulitia chumvi.

SURA YA 9

a Amu 9:28, 29

b Amu 9:30

c 1Fa 12:25

Safu ya 2

a Amu 8:33
Amu 9:4, 27

b 2Sa 11:21

46 Viongozi wote wa mnara wa Shekemu waliposikia habari hizo, wakaenda haraka katika ngome ya nyumba ya* El-berithi.^a **47** Abimeleki alipoambiwa kwamba viongozi wote wa Shekemu wamekusanyika pamoja, **48** akapanda Mlima Salmoni pamoja na watu wake. Akachukua shoka, akakata tawi la mti na kulibeba begani, akawambia hivi watu wake: "Mliyooona nikifanya, fanyeni vivyo hivyo haraka!" **49** Basi watu wote wakakata pia matawi na kumfuata Abimeleki. Kisha wakayaweka kuzunguka ile ngome na kuiteketeza. Na watu wote waliokuwa ndani ya mnara wa Shekemu wakafa pia, watu karibu 1,000, wanaueme na wanawake.

50 Kisha Abimeleki akaenda Thebesi; akalishambulia jiji la Thebesi na kuliteka. **51** Kulikuwa na mnara imara katikati ya jiji hilo, wanaume na wanawake wote, na viongozi wote wa jiji hilo wakakimbilia humo. Wakajifungia ndani yake na kupanda juu ya paa lake. **52** Abimeleki akaenda kwenye mnara huo na kuushambulia. Akaenda kwenye mlango wa mnara ili auchome moto. **53** Ndipo mwanamke fulani akaangusha jiwe la kusagia juu ya kichwa cha Abimeleki na kumpasua kichwa.^b **54** Abimeleki akamwita haraka mtumishi aliyembebea silaha na kuwambia, "Chomoa upanga wako unie, watu wasije wakasema, 'Mwanamke ndiye aliyemuua.'" Basi mtumishi wake akamchoma upanga, naye akafa.

9:46 * Au "hekalu la."

55 Wanaume Waisraeli wali-poona kwamba Abimeleki amekufa, wote wakarudi nyumbani. 56 Hivyo Mungu akalipiza kisasi kwa sababu ya uovu ambao Abimeleki alimtenda baba yake kwa kuwaua ndugu zake 70.^a 57 Pia Mungu akafanya watu wa Shekemu waadhibiwe kwa sababu ya uovu wao wote. Basi laana ya Yothamu^b mwana wa Yerubaali^c ikawapata.

10 Baada ya Abimeleki, alitokea Tola mwana wa Pua, mwana wa Dodo, wa kabila la Isakari, ili awaokoe Waisraeli.^d Aliishi Shamiri katika eneo lenye milima la Efraimu. 2 Alikuwa mwamuzi wa Waisraeli kwa miaka 23. Kisha akafa na kuzikwa huko Shamiri.

3 Baada yake akatokea Yairi Mgileadi, naye akawa mwamuzi wa Waisraeli kwa miaka 22. 4 Alikuwa na wana 30 waliopanda juu ya punda 30, nao walikuwa na majiji 30 katika nchi ya Gileadi, ambayo mpaka leo yanaitwa Hawoth-yairi.^e 5 Kisha Yairi akafa na kuzikwa huko Kamoni.

6 Waisraeli wakaanza tena kutenda maovu machoni pa Yehova,^f nao wakaanza kuabudu Mabaali,^g sanamu za Ashtorethi, miungu ya Aramu,^{*} miungu ya Sidoni, miungu ya Moabu,^h miungu ya Waamoni,ⁱ na miungu ya Wafilisti.^j Wakamwacha Yehova wala hawakuendelea kumtumikia. 7 Basi hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Waisraeli, naye akawatia mikononi mwa Wafilisti na Waamoni.^k 8 Kwa hiyo wakawatasa

SURA YA 9

a Mwa 9:6
Amu 9:5, 24

b Amu 9:7, 20

c Amu 6:32

SURA YA 10

d Amu 2:16

e Kum 3:14

f Amu 2:19
Amu 4:1
Amu 6:1
Ne 9:28g Amu 3:7
Zb 106:36-38

h Hes 25:1, 2

i 1Fa 11:5
2Fa 23:13j Amu 16:23
1Sa 5:4
2Fa 1:2k Kum 28:15, 48
Kum 31:17
Amu 2:14
Amu 4:2

Safu ya 2

a Kum 4:30

b Amu 2:13
Amu 3:7
1Sa 12:9, 10

c Kut 14:30

d Hes 21:23-25

e Amu 3:31

f Amu 2:12

g 2Nya 15:2
Mik 3:4

h 1Fa 18:27

i Yer 2:28

j Kum 7:26

k 2Nya 7:14
2Nya 33:13, 15
Zb 106:44
Isa 63:9l Mwa 19:36, 38
Amu 3:13

na kuwakandamiza sana Waisraeli mwaka huo—kwa miaka 18 waliwakandamiza Waisraeli wote waliokuwa ng'ambo ya Yordani katika nchi iliyo-kuwa ya Waamori kule Gileadi. 9 Waamoni pia walikuwa wakivuka Yordani ili kupigana na watu wa kabila la Yuda, Benjamini, na Efraimu; Waisraeli wakataabika sana. 10 Ndipo Waisraeli wakamlilia Yehova awasaidie,^a wakisema, "Tumekutendea dhambi Mungu wetu kwa sababu tumekuacha na kuabudu Mabaali."^b

11 Lakini Yehova akawaambia Waisraeli, "Je, sikuwaokoa kutoka Misri^c na kutoka mikononi mwa Waamori,^d Waamoni, Wafilisti,^e 12 Wasidoni, Waamaleki, na Wamidiani walipokuwa wakiwakandamiza? Mliponililia, niliwaokoa kutoka mikononi mwao. 13 Lakini mliniacha na kuabudu miungu mingine.^f Ndiyo sababu sitawaokoa tena.^g 14 Nendeni mkaililie miungu mliyochagua iwasaidie.^h Na iwaokoe kutoka katika taabu yenu."ⁱ 15 Lakini Waisraeli wakamwambia Yehova, "Tumetenda dhambi. Tutendee upendavyo. Lakini tunakusihii utuokoe leo hii." 16 Wakaondoa miungu ya kigeni waliyokuwa nayo na kumtumikia Yehova,^j naye hakuweza tena kuvumilia* kuwao-na Waisraeli wakiteseka.^k

17 Baadaye Waamoni^l wakakusanyika na kupiga kambi huko Gileadi. Nao Waisraeli wakakusanyika na kupiga kambi huko Mispa. 18 Ndipo wakaaji wa Gileadi na wakuu

10:16 *Au "na nafsi yake ikakosa subira kwa sababu ya."

wao wakaulizana, “Ni nani atakayetuongoza kupigana na Waamoni?”^a Atakayefanya hivyo atakuwa kiongozi wa wakaaji wote wa Gileadi.”

11 Yeftha^b Mgileadi alikuwa shujaa hodari; mama yake alikuwa kahaba na baba yake aliitwa Gileadi. **2** Lakini mke wa Gileadi pia akazaa wana. Wana hao walipokua, walimfukuza Yeftha na kumwambia, “Hutarithi chochote katika nyumba ya baba yetu kwa sababu wewe ni mwana wa mwanamke mwingine.” **3** Basi Yeftha akawa kimbia ndugu zake akaenda kuishi katika nchi ya Tobu. Na watu wanaozurura-zurura wakajiunga naye na kumfuata.

4 Baada ya muda, Waamoni wakapigana na Waisraeli.^c **5** Waamoni walipokuwa wakipigana na Waisraeli, wazee wa Gileadi wakaenda mara moja kumchukua Yeftha kutoka katika nchi ya Tobu. **6** Wakamwambia hivi Yeftha: “Njoo uwe kamanda wetu ili tupigane na Waamoni.” **7** Lakini Yeftha akawaambia wazee wa Gileadi, “Je, si ninyi mliionichukia sana na kunifukuza kutoka nyumbani mwa baba yangu?^d Kwa nini mnani-ji sasa mkiwa na matatizo?” **8** Ndipo wazee wa Gileadi wakamwambia Yeftha, “Ni kweli, lakini sasa tumerudi kwako. Ukienda pamoja nasi kupigana na Waamoni, utakuwa kiongozi wetu na wa wakaaji wote wa Gileadi.”^e **9** Ndipo Yeftha akawaambia wazee wa Gileadi, “Mkinirudisha ili nipigane na Waamoni na Yehova anisaidie kuwashinda, bila shaka nitakuwa kiongozi wenu!” **10** Wazee wa Gileadi

SURA YA 10

a Amu 11:1

SURA YA 11

b Amu 12:7
1Sa 12:11
Ebr 11:32

c Amu 10:17

d Amu 11:2

e Amu 10:18

Safu ya 2

a Amu 10:17
Amu 11:34

b Mwa 19:36, 38

c Hes 21:23, 24

d Hes 21:26

e Kum 3:16, 17

f Mwa 19:36, 37
Kum 2:9

g Kum 2:19, 37

h Hes 14:25

i Hes 20:1

j Mwa 36:1
Hes 20:14
Kum 2:4

k Mwa 19:36, 37

l Hes 20:22

m Hes 21:4

n Hes 21:11

wakamwambia Yeftha, “Yehova na awe shahidi* kati yetu na kutuhukumu tusipofanya unayosema.” **11** Basi Yeftha akaenda pamoja na wazee wa Gileadi, na watu wakamweka kuwa kiongozi na kamanda wao. Na Yeftha akasema tena masharti yake yote mbele za Yehova huko Mispa.^a

12 Kisha Yeftha akatuma wajumbe kwa mfalme wa Waamoni,^b akisema, “Nimekuko-sea nini hivi kwamba ume-kuja kuishambulia nchi yangu?” **13** Mfalme wa Waamoni akawaambia wajumbe wa Yeftha, “Nimekuja kupigana nanyi kwa sababu Waisraeli walipotoka Misri^c walichukua nchi yangu, kuanzia Arnoni^d mpaka Yaboki hadi Yordani.^e Basi sasa irudishe kwa amani.” **14** Lakini Yeftha akawatumama tena wajumbe kwa mfalme wa Waamoni **15** ili wamwambie:

“Yeftha anasema hivi: ‘Waisraeli hawakuchukua nchi ya Wamoabu^f wala nchi ya Waamoni,^g **16** kwa sababu Waisraeli walipotoka Misri, walipitia nyikani hadi Bahari Nyekundu^h na mpaka Kadeshi.ⁱ **17** Kisha Waisraeli wakatuma wajumbe kwa mfalme wa Edomu,^j wakisema, ‘Tafadhali turuhusu tupitie katika nchi yako,’ lakini mfalme wa Edomu akakataa. Kisha wakatuma wajumbe kwa mfalme wa Moabu,^k naye pia akakataa. Basi Waisraeli wakaendelea kukaa Kadeshi.^l **18** Walipopitia nyikani, waliizunguka nchi ya Edomu^m na nchi ya Moabu. Wakapitia upande wa mashariki wa nchi ya Moabuⁿ

11:10 *Tnn., “msikilizaji.”

na kupiga kambi katika eneo la Arnoni; hawakufika kwenye mpaka wa Moabu kwa sababu Mto Arnoni ulikuwa mpaka wa Moabu.^a

19 “Kisha Waisraeli wakatuma wajumbe kwa Sihoni mfalme wa Waamori, mfalme wa Heshboni, wakamwambia hivi: “Tafadhali, turuhusu tupitie katika nchi yako twende katika nchi yetu.”^b

20 Lakini Sihoni hakuwaruhusu Waisraeli wapitie katika eneo lake kwa sababu hakuwaamini, basi Sihoni akawakusanya watu wake na kupiga kambi huko Yahazi na kupigana na Waisraeli.^c **21** Kwa hiyo Yehova Mungu wa Israeli akamtia Sihoni na watu wake wote mikononi mwao, Waisraeli wakawashinda na kumiliki nchi yote ya Waamori, wakaaji wa nchi hiyo.^d **22** Basi wakamiliki eneo lote la Waamori kutoka Arnoni mpaka Yaboki na kuanzia nyikani mpaka Yordani.^e

23 “Yehova Mungu wa Israeli ndiye aliyewafukuza Waamori kutoka mbele ya watu wake Israeli,^f na sasa je, unataka kuwafukuza Waisraeli? **24** Je, humiliki nchi yoyote unayopewa na mungu wako Kemoshi?^g Basi kila mtu ambaye Yehova Mungu wetu amemfukuza kutoka mbele yetu, ndiye tutakayemfukuza.^h **25** Je, una nguvu kuliko Balakiⁱ mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu? Yeye hakushindana na Waisraeli wala kupigana nao. **26** Waisraeli walipokuwa wakikaa katika jiji la Heshboni na miji yake,^{*j} Aroeri na miji yake, na

11:26 *Au “miji jirani.”

SURA YA 11

a Hes 21:13

b Hes 21:21-26
Kum 2:26, 27

c Kum 2:32, 33

d Yos 13:15, 21

e Kum 2:36

f Ne 9:22

g 1Fa 11:7

h Kut 23:28
Kut 34:11
Hes 33:53
Kum 9:5
Kum 18:12

i Hes 22:2, 3
Yos 24:9

j Hes 21:25

Safu ya 2

a Hes 21:26

b Isa 33:22

c Amu 3:9,10
Zek 4:6

d Amu 10:17

e Kum 23:21

f 1Sa 1:11

g 1Sa 1:24

h Amu 10:17
Amu 11:11

katika majiji yote yaliyo ukiongoni mwa Mto Arnoni kwa miaka 300, kwa nini hamkuyakomboo wakati huo?^a **27** Si jakukosea, lakini umenikosea kwa kunishambulia. Yehova ambaye ni Mwamuzi^b na aamue leo kati ya Waisraeli na Waamoni.”

28 Lakini mfalme wa Waamoni hakusikiliza ujumbe wa Yeftha.

29 Roho ya Yehova ikamjia Yeftha,^c naye akapitia Gileadi na Manase na kufika Misper kule Gileadi,^d na kutoka Misper akaenda kupigana na Waamoni.

30 Ndipo Yeftha akaweka nadhiri^e kwa Yehova akisema, “Ukiwatia Waamoni mikononi mwangu, **31** yeyote atakayetoka nje ya mlango wa nyumba yangu ili kunipokea nitakaporudi baada ya kuwashinda Waamoni atakuwa wa Yehova,^f nami nitamtoa kama dhabihu ya kuteketezwa.”^g

32 Basi Yeftha akaenda kupigana na Waamoni, na Yehova akawatia mikononi mwake. **33** Akawaua watu wengi kutoka Aroeri mpaka Minithi, majiji 20, mpaka Abeleramimu. Kwa hiyo Waamoni wakashindwa na Waisraeli.

34 Mwishowe Yeftha akafika nyumbani kwake Misper,^h na tazama! binti yake akatoka ili kumpokea, huku akipiga tari na kucheza dansi! Naye alikuwa ndiye mtoto pekee. Yeftha hakuwa na mwana wala binti mwingine ila yeye.

35 Yeftha alipomwona, akararua mavazi yake na kusema, “Ole wangu, binti yangu! Umenivunja moyo,^{*i} kwa kuwa ni-

11:35 *Tnn., “Umenishusha chini sana.”

mesababisha uende mbali. Ni-metoa ahadi kwa Yehova, na siwezi kuivunja.”^a

36 Lakini akamwambia, “Baba yangu, ikiwa umetoa ahadi kwa Yehova, nitendee kama ulivyoahidi,^b kwa kuwa Yehova amelipiza kisasi dhidi ya maadui wako, Waamoni.”

37 Kisha akamwambia baba yake, “Naomba jambo hili: Niruhusu niwe peke yangu kwa miezi miwili, acha niende milimani nikaulilie ubikira wangu pamoja na wasichana wenzangu.”^{*}

38 Ndipo akamwambia, “Nenda!” Basi akamruhusu aende kwa miezi miwili, akaenda milimani pamoja na wasichana wenzake kuulilia ubikira wake.

39 Baada ya miezi miwili, akarudi kwa baba yake, kisha baba yake akatimiza nadhiri aliyoweka kumhusu.^c Hakufanya ngono na mwanamume yeyote. Basi kukawa na desturi* hii katika Israeli: **40** Kila mwaka, wasichana Waisraeli walienda kumpongeza binti ya Yeftha Mgileadi siku nne kwa mwaka.

12 Watu wa kabila la Efraimu wakaitwa, nao wakavuka na kufika Zafoni,* wakamuuliza Yeftha, “Kwa nini hukutuita ulipovuka kwenda kupigana na Waamoni?^d Tutakuteketeza pamoja na nyumba yako.” **2** Lakini Yeftha akawaambia, “Mimi na watu wangu tulikuwa na ugomvi mkubwa pamoja na Waamoni. Nikawaomba ninyi mnisaidie, lakini hamkuniokoa kutoka mikononi mwao. **3** Nili-

11:37 *Au “nikalie pamoja na rafiki zangu kwa sababu sitaolewa kamwe.”

11:39 *Au “sheria.” 12:1 *Au labda, “wakavuka kuelekea kaskazini.”

SURA YA 11

a Hes 30:2
Zb 15:4
Mhu 5:4

b Amu 11:30, 31

c 1Sa 1:22, 24

SURA YA 12

d Amu 8:1

Safu ya 2

a Amu 11:29

b Kum 3:12, 13

c Amu 3:28
Amu 7:24

d Amu 2:16

poona kwamba hamji kunio-koa, nikaamua kuhatarisha uhai wangu* na kwenda kupigana na Waamoni,^a na Yehova akawatia mikononi mwangu. Basi kwa nini mmekuja kupigana nami leo?”

4 Ndipo Yeftha akawakusanya watu wote wa Gileadi,^b wakapigana na watu wa Efraimu; na watu wa Gileadi wakawashinda Waefraimu kwa kuwa walisema, “Ninyi watu wa Gileadi ni wakimbizi tu kutoka Efraimu na kutoka Manase.” **5** Watu wa Gileadi wakateka vivuko vya Yordani^c ili kuwazuia Waefraimu wasivuke; na Waefraimu waliokuwa wakikimbia waliposema: “Naomba nivuke”; watu wa Gileadi walimuuliza kila mmoja wao, “Wewe ni Mwefraimu?” Aliposema: “Hapana!” **6** walimwambia, “Tafadhali sema Shiboletih.” Lakini alisema, “Shiboletih,” kwa kuwa hange-weza kutamka neno hilo kwa usahihi. Kwa hiyo walimkamata na kumuua kwenye vivuko vya Yordani. Basi Waefraimu 42,000 wakauawa wakati huo.

7 Yeftha alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka sita, kisha Yeftha Mgileadi akafa na kuzikwa katika jiji lake kule Gileadi.

8 Baada yake, Ibzani kuto-ka Bethlehemu akawa mwamuzi wa Israeli.^d **9** Alikuwa na watoto wa kiume 30 na wa kike 30. Akawaoza binti zake 30 nje ya ukoo wake, na akaleta wanawake 30 kutoka nje ya ukoo wake ili waolewe na watoto wake wa kiume. Alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa

12:3 *Au “Niliweka nafsi yangu mikononi mwangu.”

miaka saba. **10** Kisha Izbani akafa na kuzikwa Beth-lehemu.

11 Na baada yake, Eloni Mzabuloni akawa mwamuzi wa Israeli kwa miaka kumi. **12** Kisha Eloni Mzabuloni akafa na kuzikwa Aiyaloni katika nchi ya Zabuloni.

13 Na baada yake, Abdoni mwana wa Hileli Mpirathoni akawa mwamuzi wa Israeli. **14** Alikuwa na wana 40 na wajukuu 30 waliopanda juu ya punda 70. Alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka minane. **15** Kisha Abdoni mwana wa Hileli Mpirathoni akafa na kuzikwa Pirathoni katika nchi ya Efraimu katika mlima wa Wmamaleki.^a

13 Waisraeli wakaanza tena kutenda maovu machoni pa Yehova,^b na Yehova akawatia mikononi mwa Wafilisti^c kwa miaka 40.

2 Basi, kulikuwa na mtu mmoja huko Sora^d wa kabila la Dani^e aliyelitwa Manoa.^f Mke wake alikuwa tasa.^g **3** Siku moja malaika wa Yehova akamtokea mwanamke huyo na kumwambia, "Wewe ni tasa na huna mtoto. Lakini utapata mimba na kuzaa mwana."^h

4 Kwa hiyo, uwe mwangalifu usinywe divai wala chochote chenye kileo,ⁱ na usile kitu chochote kisicho safi.^j **5** Tazama! Utapata mimba na kuzaa mwana; na hakuna wembe utakaogusa kichwa chake^k kwa sababu mtoto huyo atakuwa Mnadhiri wa Mungu tangu kuzaliwa,^{*} naye atawaokoa Waisraeli kutoka mikononi mwa Wafilisti."^l

13:5, 7 *Tnn., "kutoka tumboni."

SURA YA 12

a Mwa 36:12
Kut 17:16
Hes 13:29
1Sa 15:2

SURA YA 13

b Amu 2:11, 19
Amu 10:6

c Yos 13:1-3
Amu 10:7

d Yos 15:20, 33
Yos 19:41, 48

e Mwa 49:16

f Amu 16:31

g Mwa 30:22, 23

h Mwa 18:10
1Sa 1:20
Lu 1:11, 13

i Hes 6:2, 3
Lu 1:15

j Law 11:26, 27

k Hes 6:2, 5

l Amu 2:16
Amu 13:1
Ne 9:27

Safu ya 2

a Amu 13:17, 18

b Amu 13:3

c Amu 13:8

d Amu 13:4

6 Ndipo mwanamke huyo akaenda na kumwambia hivi mume wake: "Mtu fulani wa Mungu wa kweli alinjia, na alikuwa kama malaika wa Mungu wa kweli, naye alikuwa mwenye kuogopesha sana. Sikumuuliza alikotoka, wala hakuambia jina lake."^a **7** Lakini aliniambia, "Tazama! Utapata mimba na kuzaa mwana. Basi usinywe divai wala chochote chenye kileo, wala usile kitu chochote kisicho safi, kwa sababu mtoto huyo atakuwa Mnadhiri wa Mungu tangu kuzaliwa^{*} mpaka kufa kwake."

8 Manoa akamsihi Yehova akisema, "Nakuomba Yehova. Tafadhali, tunaomba yule mtu wa Mungu wa kweli uliyekuwa umemtuma hivi punde arudi ili atufundishe jinsi ya kumlea mtoto atakayezaliwa."^b **9** Basi Mungu wa kweli akamsikiliza Manoa, na yule malaika wa Mungu wa kweli akamjia tena huyo mwanamke alipokuwa ameketi shambani; lakini Manoa mume wake hakuwepo. **10** Mwanamke huyo akakimbia haraka na kumwambia mume wake, "Yule mtu aliyenjia siku ile amenitokea tena."^b

11 Kwa hiyo Manoa akaondoka na kufuatana na mke wake. Akaja kwa mtu huyo na kumuuliza, "Ni wewe uliyezungumza na mke wangu?" naye akajibu: "Ni mimi."^c **12** Ndipo Manoa akasema, "Maneno yako na yatimie! Mtoto huyo ataishi maisha ya aina gani, naye atafanya kazi gani?"^c **13** Basi malaika wa Yehova akamwambia hivi Manoa: "Mke wako na ajepushe na kila kitu nilichomtaja."^d **14** Asile kitu chochote kina-

chotokana na mzabibu, asinywe divai wala chochote chenye kileo,^a na asile kitu chochote kisicho safi.^b Anapaswa kuzingatia mambo yote niliyomwagiza.”

15 Sasa Manoa akamwambia malaika wa Yehova, “Tafadhali kaa kidogo, tukuandalie mwanambuzi.”^c **16** Lakini malaika wa Yehova akamwambia Manoa, “Hata nikikaa, sitakula chakula chenu; lakini ukipenda unaweza kuki-toa kwa Yehova kuwa dhahibu ya kuteketewa.” Manoa hakujua kwamba mtu huyo alikuwa malaika wa Yehova. **17** Kisha Manoa akamuuliza malaika wa Yehova, “Unaitwa nani,^d ili neno lako litakapotimia tukuheshimu?” **18** Hata hivyo, malaika wa Yehova akamwambia: “Kwa nini unataka kujua jina langu, wakati jina lenyewe ni la ajabu?”

19 Basi Manoa akachukua mwanambuzi na toleo la nafaka, akamtolea Yehova juu ya mwamba. Naye akafanya jambo la kushangaza huku Manoa na mke wake wakitazama. **20** Mwali wa moto ulipokuwa ukipaa kuelekea mbinguni, malaika wa Yehova akapaa katika huo mwali uliotoka katika madhabahu huku Manoa na mke wake wakitazama. Basi wakaanguka chini kifudufudi. **21** Malaika wa Yehova hakumtokea tena Manoa na mke wake. Ndipo Manoa akatambua kwamba huyo alikuwa malaika wa Yehova.^e **22** Kisha Manoa akamwambia hivi mke wake: “Hakika tutakufa, kwa sababu tumemwona Mungu.”^f **23** Lakini mke wake akamwambia, “Kama Yehova angetaka kutuua, hangekuba-

SURA YA 13

a Hes 6:2, 3

b Law 11:26, 27

c Mwa 18:5, 7
Amu 6:18, 19
Ebr 13:2

d Mwa 32:29
Amu 13:6

e Amu 6:22, 23

f Kut 33:20
Yoh 1:18

Safu ya 2

a Amu 13:16

b Ebr 11:32

c Amu 3:9, 10
Amu 6:34
Amu 11:29
1Sa 11:6

d Amu 18:11, 12

e Yos 15:20, 33

SURA YA 14

f Kum 7:3

g Amu 13:1

li dhahibu ya kuteketewa^a na toleo la nafaka kutoka mikononi mwetu, naye hangetuonyesha mambo haya yote, wala hangetuambia mambo haya yote.”

24 Baadaye mwanamke huyo akazaa mwana na kumpa jina Samsoni;^b na mvulana huyo akazidi kukua, na Yehova akaendelea kumbariki. **25** Baada ya muda roho ya Yehova ikaanza kumchochea^c huko Mahane-dani^d kati ya Sora na Eshtaoli.^e

14 Ndipo Samsoni akaenda Timna, na akiwa huko akamwona mwanamke Mfilisti.* **2** Basi akarudi na kuwaambia hivi wazazi wake: “Nimevutiwa na mwanamke fulani Mfilisti huko Timna, ninaomba mniletee awe mke wangu.” **3** Lakini baba yake na mama yake wakamwambia, “Je, huwezi kupata mke kati ya watu wetu wa ukoo na kati ya ndugu zetu wote?^f Je, ni lazima uoe mke kutoka kati ya Wafilisti wasiotahiriwa?” Lakini Samsoni akamwambia baba yake, “Niletee mwanamke huyo, kwa sababu ndiye anayenifaa.”* **4** Lakini wazazi wake hawakujua kwamba Yehova aliongoza jambo hilo, kwa sababu Alikuwa akitafuta nafasi ya kuwapiga Wafilisti, kwa kuwa Wafilisti walikuwa wakiwatawala Waisraeli wakati huo.^g

5 Basi Samsoni akaenda na baba yake na mama yake hadi Timna. Alipofika katika mashamba ya mizabibu ya Timna, simba* akamjia akinguruma.

14:1 *Tnn., “mwanamke wa binti za Wafilisti.” **14:3** *Tnn., “anafaa machoni pangau.” **14:5** *Au “mwanasimba mwenye manyoya marefu shingoni.”

6 Ndipo roho ya Yehova ikamtia nguvu,^a naye akampasua simba huyo vipande viwili, kama mtu anavyompasua mwanambuzi kwa mikononyake. Lakini hakumwambia baba yake au mama yake jambo alilofanya. 7 Kisha akaenda kuzungumza na yule mwanamke, na bado Samsoni aliona kwamba anamfaa.^b

8 Baadaye alipokuwa akirudi kumchukua mwanamke huyo aende naye nyumbani,^c alienda kuangalia ule mzoga wa simba, nao ulikuwa na nyuki wengi na asali. 9 Basi akakwangua asali hiyo na kuitia mikononi mwake, akaila huku akitembea. Alipomfikia baba yake na mama yake, akawagawia ili wale. Lakini hakuwambia kwamba alikwangua kutoka katika mzoga wa simba.

10 Na baba yake akaenda kumwona yule mwanamke, naye Samsoni akafanya karamu huko, kwa maana hivyo ndivyo vijana wa kiume walivyokuwa wakifanya. 11 Na watu walipomwona, wakamletea vijana 30 wa kuandamana naye. 12 Kisha Samsoni akawaambia, "Nina kitendawili. Mkikitegua katika siku saba za karamu, nitawapa mavazi 30 ya kitani na mavazi mengine 30. 13 Lakini mkishindwa kukitegua, mtanipa mavazi 30 ya kitani na mavazi mengine 30." Wakamwambia, "Tega kitendawili chako, tusikie." 14 Basi akawaambia,

"Mlo ulitoka katika mlaji,

Na kitu kitamu kilitoka
kwa mwenye nguvu."^d

Nao hawakuweza kutegua kitendawili hicho kwa siku tatu. 15 Siku ya nne waka-

SURA YA 14

a Amu 13:24, 25

b Amu 14:2

c Mwa 24:67
Mt 1:24

d Amu 14:8, 9

Safu ya 2

a Amu 16:5

b Amu 16:15

c Amu 16:16, 18

d Amu 14:14

e Amu 14:15

f Amu 13:24, 25
Amu 14:6
Amu 15:14g Yos 13:2, 3
Amu 1:18

h Amu 14:12

mwambia hivi mke wa Samsoni: "Mshawishi mume^a wako ili atutegulie kitendawili hicho. Kama sivyo, tutakuteketeza kwa moto pamoja na watu wa nyumba ya baba yako. Je, mlitualika hapa ili mchukue mali zetu?"

16 Basi mke wa Samsoni akamlilia na kusema, "Hakika unanichukua; hunipendi.^b Uliwategea watu wangu kitendawili, lakini hujaniambia maana yake." Samsoni akamwambia, "Hata sijamwambia baba yangu wala mama yangu! Nikwambie wewe?" 17 Lakini akaendelea kumlilia siku zilizobaki za karamu hiyo ya siku saba. Hatimaye Samsoni akamteguulia kitendawili hicho katika siku ya saba, kwa sababu alimsumbua sana. Ndipo mwanamke huyo akawaambia watu wake maana ya kitendawili hicho.^c 18 Basi siku ya saba kabla ya jua kutua,^{*} wanaume wa jiji hilo wakamwambia hivi Samsoni:

"Ni nini kitamu kuliko
asali,

Na ni nani mwenye nguvu
kuliko simba?"^d

Akawaambia:

"Kama hamngelima
na ng'ombe wangu
mchanga,^e

Hamngekitegua kitendawili
changu."^f

19 Kisha roho ya Yehova ikamtia nguvu,^f akaenda Ashkeloni,^g akawaua watu 30, akachukua mavazi yao na kuwapa watu waliotegua kiteendawili.^h Akarudi nyumbani kwa baba yake akiwa amekasirika sana.

14:18 * Au labda, "kabla hajaingia katika chumba cha ndani."

20 Kisha wakamchukua mke wa Samsoni^a na kumpa mmoja wa wale vijana walioandamana naye.^b

15 Baada ya muda, wakati wa mavuno ya ngano, Samsoni alimchukua mwanambuzi na kwenda kumtembelea mke wake. Akasema: "Ningependa kuingia nikamwone mke wangu katika chumba cha kulala."* Lakini baba ya mwanamke huyo hakumruhusu kuingia. **2** Baba ya mwanamke huyo akasema, "Nilidhani, 'Hakika unamchukua.'"^c Kwa hiyo nikampa kijana mwenzako.^d Dada yake mdogo ni mrembo kuliko yeye. Tafadhali, mchukue huyo badala yake." **3** Hata hivyo, Samsoni akawaambia, "Wakati huu Wafilisti hawatani laumu nikiwadhuru."

4 Basi Samsoni akaenda na kuwakamata mbweha 300. Kisha akachukua miennege, akawafunga mikia wawili-wawili na kuweka mwenge mmoja kati ya kila mikia miwili. **5** Halafu akaiwasha moto ile miennege na kuwaachilia mbweha hao waingie katika mashamba ya nafaka ya Wafilisti. Basi akateketeza kila kitu kuanzia masuke mpaka nafaka iliyo shambani, na pia mashamba ya mizabibu na ya mizeituni.

6 Wafilisti wakauliza: "Ni nani aliyefanya hivi?" Wakambiwa: "Ni Samsoni, mkwe wa yule Mtimna, kwa sababu alimchukua mke wa Samsoni na kumpa kijana mwenzake."^e Kwa hiyo Wafilisti wakaenda na kumteketeza mwanamke huyo na baba yake.^f **7** Kisha

15:1 *Au "chumba cha ndani."

SURA YA 14

a Amu 14:2

b Amu 14:11
Amu 15:1, 2

SURA YA 15

c Amu 14:17

d Amu 14:11, 20

e Amu 14:11, 20

f Amu 14:15

Safu ya 2

a Amu 14:4

b 2Sa 23:11, 12

c Amu 13:1

d Amu 13:24, 25
Amu 14:5, 6

Samsoni akawaambia, "Kama haya ndiyo mambo mnayofanya, sitawaacha mpaka nitakapolipiza kisasi."^a **8** Basi akawapiga na kuwaua watu wengi, mmoja baada ya mwingine, kisha akashuka na kwenda kukaa pangoni katika mwamba wa Etamu.

9 Baadaye Wafilisti wakapanda na kupiga kambi kule Yuda, nao walikuwa wakizunguka-zunguka katika mji wa Lehi.^b **10** Ndipo watu wa Yuda wakawauliza, "Kwa nini mmekuja kutushambulia?" Wakajibu: "Tumekuja kumkamata* Samsoni, na kumtendea kama alivyotutendea."

11 Basi wanaume 3,000 wa Yuda wakashuka kwenye pango lililo katika mwamba wa Etamu, wakamuuliza Samsoni, "Je, hujui kwamba Wafilisti wanatutawala?"^c Kwa nini umetutendea hivi?" Akawajibu: "Nimewatendea kama walivyotendea." **12** Lakini wakawambia, "Tumekuja kukukamata* ili tukutie mikononi mwa Wafilisti." Samsoni akawaambia, "Niapieni kwamba ninyi hamtanidhuru." **13** Wakawambia, "Usiogope, tutakufunga tu na kukupeleka kwao, lakini hatutakuu."

Basi wakamfunga kwa kamba mbili mpya na kumtoa mwambani.

14 Alipofika Lehi, Wafilisti walishangilia sana kumwona. Kisha roho ya Yehova ikamtia nguvu,^d na kamba alizofungwa mikononi zikawa kama nyuzi za kitani zilizocho-mwa moto, nazo zikalegea* na kuanguka kutoka mikononi

15:10 *Au "kumfunga." 15:12 *Au "kukufunga." 15:14 *Tnn., "zikayeyuka."

mwake.^a **15** Akaona utaya mbichi wa punda dume; akauchukua na kuutumia kuua wanaume 1,000.^b **16** Kisha Samsoni akasema:

“Kwa utaya wa punda –rundo moja, marundo mawili!

Kwa utaya wa punda ni-meua wanaume 1,000.”^c

17 Baada ya kusema hayo, alitupa utaya huo na kupaita mahali hapo Ramath-lehi.^{*d}

18 Kisha akahisi kiu sana, akamlilia Yehova akisema, “Ni wewe uliyemtumia mtumishi wako kuleta ukombozi huu mkubwa. Je, sasa nife kwa kiu na kuchukuliwa na watu wasiotahiriwa?” **19** Basi Mungu akapasua mahali penye shimo huko Lehi, na maji yakatiririka kutoka humo.^e Alipoyanywa, roho yake ikamrudia* akapata nguvu tena. Ndiyo sababu aliiita sehemu hiyo Enhakore,^f nayo iko Lehi mpaka leo.

20 Samsoni alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka 20 katika siku za Wafilisti.^f

16 Siku moja Samsoni alienda Gaza, akamwona kahaba fulani na kuingia nyumbani mwake. **2** Watu wa Gaza wakaambiwa, “Samsoni ameingia humu.” Basi wakamzingira na kumvizia usiku kucha kwenye lango la jiji. Wakakaa kimya usiku kucha, wakisema miongoni mwao, “Kesho asubuhi tutamuua.”

3 Lakini Samsoni akaendelea kulala mpaka usiku wa manane. Kisha akaamka na kung’oa malango ya jiji pamoja

15:17 *Maana yake “Kilima cha Utaya.”

15:19 *Au “nguvu zake zikamrudia.”

^fMaana yake “Chemchemi ya Anayeita.”

SURA YA 15

a Amu 16:9,12

b Amu 3:31

c Amu 16:30

d Amu 15:9

e Kut 17:6

f Mwa 49:16
Amu 2:16
Amu 13:1, 5
Amu 16:31
Ebr 11:32

Safu ya 2

SURA YA 16

a Amu 16:18

b Amu 14:15

c Amu 15:14

na miimo yake miwili na ko-meo. Akajitwika mabegani na kuipeleka kwenye kilele cha mlima ulio karibu na Hebroni.

4 Baada ya hayo akampenda mwanamke fulani katika Bonde* la Soreki, aliyetwa Delila.^a **5** Basi watawala wa Wafilisti wakaenda kwa mwanamke huyo na kumwambia, “Mdanganye*^b ili ujue chanzo cha nguvu zake nyingi na jinsi tunavyoweza kumshinda, kumfunga, na kumdhibiti. Na kila mmoja wetu atakupa vipande 1,100 vya fedha.”

6 Baadaye Delila akamwambia Samsoni, “Naomba uniambie chanzo cha nguvu zako nyingi na kitu kinachoweza kutumiwa kukufunga na kukudhibiti.” **7** Samsoni akamwambia, “Wakinifunga kwa kamba saba mbichi za upinde, nitakuwa dhaifu kama mwanadamu mwingine yeyote.”

8 Basi watawala wa Wafilisti wakamletea mwanamke huyo kamba saba mbichi za upinde, akamfunga nazo. **9** Nao wakawaficha watu fulani katika chumba cha ndani ili wamvizie, basi Delila akamwambia, “Wafilisti wamekuja kukushambulia, Samsoni!” Ndipo akazikata hizo kamba kwa urahisi kama uzi wa kitani unavyokatika unapoguswa na moto.^c Nao hawakujua siri ya nguvu zake.

10 Basi Delila akamwambia Samsoni: “Umenihadaa* na kunidanganya. Sasa tafadhali, niambie unaweza kufungwa kwa kitu gani?” **11** Kwa hiyo akamwambia, “Wakinifunga kwa kamba mpya ambazo hazijatumiwa,

16:4 *Au “Korongo.” 16:5 *Au “Mshawishi.” 16:10 *Au “Umenichezea.”

nitakuwa dhaifu kama wanaadamu mwingine yeyote.”

12 Basi Delila akachukua kamba mpya akamfunga nazo, kisha akamwambia hivi Samsoni kwa sauti kubwa: “Wafilisti wamekuja kukushambulia, Samsoni!” (Wakati huo watu waliokuwa wakimvizia wali kuwa wamejificha katika chumba cha ndani.) Ndipo akazikata kamba hizo kutoka mikononi mwake kama nyuzi.^a

13 Kisha Delila akamwambia Samsoni, “Mpaka sasa umenihadaa na kunidanganya.^b Niambie unaweza kufungwa kwa kitu gani?” Akamjibu, “Kwa kufuma vishungi saba vya nywele zangu kwa uzi wa mtande.” **14** Basi akavifunga kwa kigingi na kumwambia hivi kwa sauti kubwa: “Wafilisti wamekuja kukushambulia, Samsoni!” Basi akaamka kutoka usingizini na kung’oa kigingi hicho cha wafumaji na uzi wa mtande.

15 Sasa Delila akamwambia, “Unawezaje kusema ‘Nakupenda’^c wakati moyo wako haupo pamoja nami? Umenihadaa mara tatu na hujaniambia chanzo cha nguvu zako nyingi.”^d **16** Delila alimsumbua Samsoni siku baada ya siku na kumshinikiza, akamchosa* hivi kwamba akatamani kufa.^e **17** Mwishowe akamfunulia moyo wake na kumwambia, “Kichwa changu hakijawahi kamwe kuguswa na wembe, kwa kuwa mimi ni Mnadhiri wa Mungu tangu kuzaliwa.”^f Nikinyolewa, nguvu zangu zitanitoka, nami nita-

16:16 *Au “nafsi yake ikachoka.” **16:17** *Tnn., “kutoka tumboni mwa mama yangu.”

SURA YA 16

a Amu 16:9

b Amu 16:7,11

c Amu 14:16

d Amu 16:7
Amu 16:11
Amu 16:13

e Amu 14:17

f Hes 6:5
Amu 13:5,7

Safu ya 2

a Amu 16:5

b Amu 16:9
Amu 16:12
Amu 16:14

c Amu 13:5

d 1Sa 5:4

e Amu 15:4, 5

f Amu 15:7,8
Amu 15:15, 16

kuwa dhaifu kama wanadamu wengine wote.”

18 Delila alipoona kwamba Samsoni amemfunulia moyo wake, akawaita mara moja watawala wa Wafilisti^a na kuwaambia, “Njooi, kwa maana sasa amenifunulia moyo wake.” Basi watawala wa Wafilisti wakaja kwa Delila wakiwa na zile pesa. **19** Delila akamlaza Samsoni mapajani; akamwita mtu ili amnyoe vile vishungi saba vya nywele zake. Ndipo Delila akaanza kumdhibiti, kwa maana alikuwa akiishiwa na nguvu. **20** Kisha Delila akamwambia hivi kwa sauti kubwa: “Wafilisti wamekuja kukushambulia, Samsoni!” Ndipo akaamka kutoka usingizini na kusema, “Nitatoka nje kama awali^b na kujinasua.” Lakini hakujua kwamba Yehova alikuwa amemwacha. **21** Basi Wafilisti wakamkamata na kumng’oa macho. Wakampeleka Gaza na kumfunga kwa pingu mbili za shaba, akawa akisaga nafaka gerezani. **22** Lakini nywele za kichwa chake zikaanza kukua tena baada ya kunyolewa.^c

23 Watawala wa Wafilisti wakakusanyika ili kusherehekea na kumtolea dhahihu nyingi mungu wao Dagoni,^d kwa kuwa walisema, “Mungu wetu amemia mikononi mwetu adui yetu Samsoni!” **24** Watu walipomwona, wakamsifu mungu wao wakisema, “Mungu wetu amemia mikononi mwetu adui yetu aliyeharibu nchi yetu^e na kuua watu wengi kati yetu.”^f

25 Mioyo yao ilipojaa furaha wakasema, “Mwiteni Samsoni atutumbuize.” Basi

wakamwita Samsoni kuto-ka gerezani ili awatumbuize; wakamsimamisha katikati ya nguzo. **26** Samsoni akamwambia hivi mvulana aliyekuwa amemshika mkono: “Niache niguse nguzo zinazotegemeza nyumba hii, ili niziegemee.” **27** (Basi nyumba hiyo ilikuwa imejaa wanaume na wana-wake. Na watawala wote wa Wafilisti walikuwemo, na dari-ni kulikuwa na watu wapa-tao 3,000, wanaume na wana-wake, waliokuwa wakimtaza-ma Samsoni akiwatumbuiza.)

28 Ndipo Samsoni^a akamli-lia Yehova akisema, “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ni-kumbuke, tafadhali, na kuni-tia nguvu,^b tafadhali, mara hii moja tu, Ee Mungu, acha ni-walipize kisasi Wafilisti kwa ajili ya jicho moja tu, kati ya ma-cho yangu mawili.”^c

29 Kisha Samsoni akazishi-ka nguzo mbili za katikati zil-lizotegemeza nyumba hiyo, nguzo moja kwa mkono wa ku-lia na ile nyingine kwa mko-no wa kushoto. **30** Kisha Sa-msoni akasema hivi kwa sauti kubwa: “Acha nife* pamoja na Wafilisti!” Ndipo akasukuma nguzo hizo kwa nguvu zake zote, na nyumba hiyo ika-waangukia watawala na watu wote waliokuwemo.^d Kwa hiyo watu aliowau wakati wa kifo chake walikuwa wengi kuliko aliowaua maishani mwake.^e

31 Baadaye ndugu zake na watu wote wa familia ya baba yake wakaja kumchukua. Wakamzika kati ya Sora^f na Eshtaoli katika kaburi la Ma-noa^g baba yake. Samsoni ali-kuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka 20.^h

16:30 *Au “nafsi yangu ife.”

SURA YA 16

a Ebr 11:32

b Amu 14:5, 6
Amu 14:19
Amu 15:14

c Amu 16:21

d Amu 16:27

e Amu 14:19
Amu 15:7, 8
Amu 15:15, 16

f Amu 13:2

g Amu 13:8

h Amu 2:16
Amu 15:20

Safu ya 2

SURA YA 17

a Yos 17:14, 15

b Kut 20:4
Law 26:1
Kum 27:15c Kut 28:6
Amu 8:27

d Mwa 31:19

e Hes 3:10
Kum 12:11, 13
2Nya 13:8, 9

f 1Sa 8:4, 5

g Amu 21:25

h Mik 5:2

i Hes 3:45
Yos 14:3
Yos 18:7

17 Kulikuwa na mtu mmoja katika eneo lenye mili-ma la Efraimu^a aliyelitwa Mika. **2** Siku moja alimwambia hivi mama yake: “Vile vipande 1,100 vya fedha ulivyoibiwa na ukamlaani aliyekuibia, nikiwa nasikia—mimi ndiye niliyevi-chukua.” Mama yake akamw-ambia, “Yehova na akubariki mwanangu.” **3** Basi akamru-dishia mama yake vile vipande 1,100 vya fedha, lakini mama yake akasema, “Nitazitakasa fedha hizi kwa ajili ya Yeho-va zitoke mikononi mwangu ili mwanangu azitumie kutenge-neza sanamu ya kuchongwa na sanamu ya chuma.*^b Sasa nakurudishia fedha hizi.”

4 Baada ya kumrudishia mama yake fedha hizo, mama yake akachukua vipande 200 vya fedha na kumpa mfua fe-dha. Naye akatengeneza sana-mu ya kuchongwa na sanamu ya chuma;* na sanamu hizo zikawekwa katika nyumba ya Mika. **5** Na Mika alikuwa na nyumba ya miungu, naye akatengeneza efodi*^c na sana-mu za terafimu*^d na kumweka mmoja wa wanawe awe kuha-ni wake.^e **6** Siku hizo haku-kuwa na mfalme katika Israe-li.^f Kila mtu alifanya jambo ali-loona ni jema machoni pake.*^g

7 Basi kulikuwa na kija-na fulani kutoka Bethlehemu^h kule Yuda aliyetoka katika ukoo wa Yuda. Alikuwa Mlawi/ na alikuwa ameishi huko kwa muda. **8** Kijana huyo akaon-doka katika jiji la Bethlehe-mu katika nchi ya Yuda ili ata-fute mahali pengine pa kui-shi. Alipokuwa akisafiri, ali-

17:3, 4 *Au “sanamu ya kuyeyushwa.”
17:5 *Au “kizibao cha kuhani.” *Au
“miungu ya familia; sanamu.” 17:6
*Au “alilofikiri linafaa.”

fika katika eneo lenye milima la Efraimu, katika nyumba ya Mika.^a **9** Mika akamuuliza, “Unatoka wapi?” Akamjibu, “Mimi ni Mlawi kutoka Bethlehemu kule Yuda, natafuta mahali pa kuishi.” **10** Basi Mika akamwambia, “Kaa pamoja nami, uwe kama baba* na kuhani wangu. Nitakupa vipande kumi vya fedha kwa mwaka, mavazi, na chakula.” Kwa hiyo Mlawi huyo akaingia nyumbani mwake. **11** Mlawi huyo akakubali kukaa na Mika, naye akawa kama mmoja wa wana-we. **12** Isitoshe, Mika akamweka Mlawi huyo kuwa kuhani wake,^b akaishi nyumbani mwa Mika. **13** Basi Mika akasema, “Sasa najua kwamba Yehova atanitendea mema, kwa maana Mlawi amekuwa kuhani wangu.”

18 Siku hizo hakukuwa na mfalme katika Israeli.^c Na siku hizo watu wa kabila la Dani^d walikuwa wakitafuta mahali pa kukaa, kwa sababu kufikia wakati huo hawakuwa wamepata urithi miongoni mwa makabila ya Israeli.^e

2 Watu wa kabila la Dani wakawatuma wanaume wata-no mashujaa kutoka miongoni mwao, waliotoka Sora na Eshtaoli,^f ili waipeleleze nchi na kuichunguza. Wakawambia, “Nendeni mkaichunguze nchi.” Walipofika kwenye eneo lenye milima la Efraimu, nyumbani kwa Mika,^g wakalala huko usiku huo. **3** Walipokaribia nyumba ya Mika, walimsikia* yule kijana na kutambua kwamba alikuwa Mlawi, basi wakaenda kumuuliza, “Ni nani aliyekule-

17:10 *Au “mshauri.” 18:3 *Au “walitambua lafadhi ya.”

SURA YA 17

a Amu 17:1, 5

b Hes 3:10
Amu 17:5

SURA YA 18

c Amu 8:23
1Sa 8:4, 5

d Yos 19:40

e Yos 19:47, 48
Amu 1:34

f Yos 19:41, 48

g Amu 17:1, 5

Safu ya 2

a Amu 17:9, 10

b Yos 19:47, 48
Amu 18:29

c Amu 18:27

d Yos 15:20, 33
Amu 18:2

e Amu 18:7, 27

f Kut 3:8
Kum 8:7-9

g Amu 18:2

h 1Sa 7:1

i Amu 13:24, 25

ta huku? Unafanya nini hapa? Ni kazi gani iliyokuleta hapa?”

4 Akawaeleza mambo ambayo Mika alimtendea na kuwambia, “Ameniajiri ili niwe kuhani wake.”^a **5** Ndiyo wakamwambia, “Tafadhali, muulize Mungu ikiwa safari yetu itafanikiwa.” **6** Kuhani huyo akawambia, “Nendeni kwa amani. Yehova yuko pamoja nanyi katika safari yenu.”

7 Basi wanaume hao wata-no wakaendelea na safari na kufika Laishi.^b Wakaona jinsi wakaaji wa huko walivyoishi kama Wasidoni bila kumtegemea yeyote. Walikuwa watu watulivu wasio na wasiwasi,^c na hakukuwa na mtawala yeyote aliyewakandamiza wala kuwasumbua. Waliishi mbali sana na Wasidoni, na hawakushughulika na watu wengine.

8 Wanaume hao waliporudi kwa ndugu zao huko Sora na Eshtaoli,^d ndugu zao wakawauliza, “Mambo yaliendaje?” **9** Wakajibu, “Twendeni tukapigane nao, kwa kuwa tumona nchi yao ni nzuri sana. Kwa nini mnasitasita? Msikawie kwenda kumiliki nchi hiyo. **10** Mtakapofika, mtakuta watu wasio na wasiwasi,^e na nchi yao ni kubwa. Mungu amewapa ninyi nchi hiyo ambayo haipungukiwi na kitu chochote duniani.”^f

11 Basi wanaume 600 wa kabila la Dani wenye silaha wakatoka Sora na Eshtaoli.^g **12** Nao wakaenda na kupiga kambi karibu na Kiriath-yearimu^h kule Yuda. Ndiyo sababu eneo hilo lililo upande wa magharibi wa Kiriath-yearimu, linaitwa Mahane-daniⁱ mpaka leo.

18:12 *Maana yake “Kambi ya Dani.”

13 Wakatoka huko na kwenda kwenye eneo lenye milima la Efraimu, wakafika nyumbani kwa Mika.^a

14 Kisha wale wanaume watano waliokuwa wameenda kuipeleleza nchi ya Laishi^b wakawaambia hivi ndugu zao: “Je, mnajua kwamba nyumba hizi zina efodi,^{*} terafimu,[#] sanamu ya kuchongwa, na sanamu ya chuma?^{△c} Fiki-rieni mtakalofanya.” **15** Basi wakaenda kwenye nyumba ya yule kijana Mlawi,^d nyumbani kwa Mika, ili kumjulia hali. **16** Wakati huo, wale wanaume 600 wa kabila la Dani^e wenye silaha, walikuwa wamesimama langoni. **17** Wale wanaume watano walioenda kuipeleleza nchi^f wakaingia ndani ili kuchukua ile sanamu ya kuchongwa, ile efodi,^{*g} zile terafimu,^h na ile sanamu ya chuma.^{△i} (Yule kuhaniⁱ alikuwa amesimama langoni pamoja na wale wanaume 600 wenye silaha.) **18** Nao wakaingia katika nyumba ya Mika wakachukua ile sanamu ya kuchongwa, ile efodi,^{*} zile terafimu,[#] na ile sanamu ya chuma.[△] Kuhani huyo akawauliza, “Mnafanya nini?” **19** Lakini wakamwambia, “Nyamaza. Funika kinywa chako kwa mkono wako, tufuate ili uwe baba^{*} na kuhani wetu. Je, ni bora kwako kuwa kuhani wa nyumba ya mtu mmoja^k au kuhani wa kabila na ukoo katika Israeli?”^l **20** Ndipo kuhani huyo akari-dhika, akachukua ile efodi,^{*}

18:14, 17, 18, 20 *Au “kizibao cha kuhani.” 18:14, 17, 18, 20 #Au “miungu ya familia; sanamu.” 18:14, 17, 18 △Au “sanamu ya kuyeyushwa.” 18:19 *Au “mshauri.”

SURA YA 18

a Amu 17:1, 5

b Amu 18:2
Amu 18:29

c Kum 27:15
Amu 17:4, 5

d Amu 17:7,12
Amu 18:30

e Amu 18:11

f Amu 18:2

g Kut 28:6
Amu 8:27

h Mwa 31:19

i Law 19:4
Kum 27:15
Amu 17:3-5

j Amu 17:12

k Amu 17:12

l Amu 18:30

Safu ya 2

a Amu 17:4, 5

b Amu 18:7, 10

c Yos 19:47, 48
Amu 18:29

d Hes 13:17, 21

e Yos 19:47, 48
Amu 20:1
1Fa 4:25
1Fa 12:28, 29

zile terafimu,[#] na ile sanamu ya kuchongwa,^a akaenda nao.

21 Basi wakaanza safari yao, huku wakitanguliwa na watoto, mifugo, na vitu vyao vyenye thamani. **22** Walipokuwa umbali fulani kutoka nyumbani kwa Mika, wanau-me walioishi karibu na Mika walikusanyika pamoja, wakawafuatia na kuwafikia wale watu wa kabila la Dani. **23** Walipowapigia kelele watu wa kabila la Dani, waligeuka na kumuuliza Mika, “Una shida gani? Kwa nini umekuja na umati huu?” **24** Basi akasema, “Mmechukua miungu niliyojitengenezea na kuondoka na kuhani wangu pia. Mkani-cha bila chochote. Mnawezaje kuniuliza, ‘Una shida gani?’” **25** Ndipo wale wanaume wa kabila la Dani wakamwambia, “Usitufokee; la sivyo, wanau-me hawa wenye hasira wata-kushambulia na kukuua wewe na watu wa nyumbani mwako.” **26** Basi watu wa kabila la Dani wakaendelea na safari, na Mika alipoona kwamba wamemzidi nguvu, akageuka na kurudi nyumbani kwake.

27 Baada ya kuchukua miungu ya Mika, pamoja na kuhani wake, wakaenda kuwashambulia watu watulivu na wasio na wasiwasi^b wa Laishi.^c Wakawaua kwa upanga na kuteteza jiji lao. **28** Hawakuwa na mtu wa kuwaokoa, kwa sababu waliishi mbali sana na Wasidoni katika bonde^{*} la Beth-rehobu,^d nao hawaku-shughulika na watu wengine. Watu wa kabila la Dani wakalijenga upya jiji hilo na kishi humo. **29** Wakaliita jiji hilo Dani^e sawa na jina la baba

18:28 *Au “nchi tambarare ya chini.”

yao, Dani, mtoto wa Israeli.^a Lakini mwanzoni jiji hilo liliitwa Laishi.^b **30** Kisha watu wa kabila la Dani wakaanza kuabudu ile sanamu ya kuchongwa,^c naye Yonathani^d mwana wa Gershomu,^e mwana wa Musa, na wanawe wakawa makuhani wa kabila la Dani mpaka wakaaji walipopelekwa uhamishoni. **31** Nao wakaisimamisha ile sanamu ya kuchongwa iliyotengenezwa na Mika, na sanamu hiyo ikae ndelea kuwa huko sikuzote ambazo nyumba ya Mungu wa kweli ilikuwa Shilo.^f

19 Katika siku hizo, wakati ambapo hakukuwa na mfalme katika Israeli,^g Mlawi fulani aliyekuwa akiishi mbali katika eneo lenye milima la Efraimu^h alimwota suria kutoka Bethlehemuⁱ kule Yuda. **2** Lakini suria huyo hakuwa mwaminifu kwake, akamwacha mume wake na kurudi Bethlehemu nyumbani kwa baba yake kule Yuda. Naye akakaa huko kwa miezi minne. **3** Basi mume wake akaenda kumsihi arudi; alienda na mtumishi wake wa kiume na punda wawili. Mwanamke huyo akamkaribisha katika nyumba ya baba yake. Baba yake alifurahi kumwona. **4** Basi baba mkwe wake, yaani, baba ya yule msichana, akamshawishi akae hapo kwa siku tatu; wakala na kunywa; naye akalala huko.

5 Siku ya nne, walipoamka asubuhi na mapema ili waanze safari, baba ya yule msichana akamwambia hivi mkwe wake: "Kula chakula kidogo ili upate nguvu,* kisha uende."

19:5, 8 *Au "ili moyo wako uendelee kuishi."

SURA YA 18

a Mwa 30:6
Mwa 32:28

b Amu 18:7

c Amu 17:1, 4
Amu 18:18

d Amu 17:12

e Kut 2:21, 22

f Kut 40:2
Yos 18:1
1Sa 1:3

SURA YA 19

g 1Sa 8:4, 5

h Yos 17:14, 15

i Mwa 35:19
Mik 5:2

Safu ya 2

a Yos 15:8, 63
Yos 18:28
Amu 1:8

b Yos 18:28

6 Basi wakaketi, na wote wawili wakala na kunywa; kisha baba ya yule msichana akamwambia huyo mwanamume, "Tafadhali, lala hapa usiku huu, ustarehe."* **7** Mwanamume huyo alipotaka kuondoka, baba mkwe wake akamsihi sana abaki, naye akalala tena usiku huo.

8 Alipoamka asubuhi na mapema siku ya tano ili aende, baba ya msichana huyo akasema, "Tafadhali, kula chakula kidogo ili upate nguvu."* Nao wakakaa mpaka jioni sana, na wote wawili wakaendelea kula. **9** Yule mwanamume alipotaka kuondoka pamoja na suria* wake na mtumishi wake, baba mkwe wake, yaani, baba ya yule msichana, akamwambia, "Tazama! Mchana umekwisha, jioni inakaribia. Tafadhali, lala hapa usiku huu, ustarehe. Amkeni mapema kesho na kuanza safari yenu ya kwenda nyumbani kwenu."* **10** Hata hivyo, mwanamume huyo hakutaka kulala huko tena, basi akaondoka na kusafiri mpaka Yebusi, yaani, Yerusalemu.^a Alikuwa na punda wake wawili wenye matandiko, suria wake, na mtumishi wake.

11 Walipokaribia Yebusi, ilikuwa jioni sana. Basi yule mtumishi akamuuliza bwana wake, "Tunaweza kulala katika jiji hili la Wayebusi usiku huu?" **12** Lakini bwana wake akamjibu hivi: "Hatutalala katika jiji la watu ambao si Waisraeli. Tutaendelea na safari mpaka Gibe."* **13** Kisha akamwambia hivi mtumishi

19:6 *Au "uchangamshe moyo wako."
19:9 *Au "mke." *Tnn., "katika hema lenu."

wake: “Twende, tujitahidi kufika Gibea au Rama; tulale katika mojawapo ya majiji hayo.”^a **14** Basi wakaendelea na safari, na jua likaanza kutua walipokaribia Gibea, jiji la Wabenjamini.

15 Wakaingia Gibea ili walale humo usiku. Wakaketi katika uwanja wa jiji, lakini hakuna yeyote aliyewakaribisha ili walale nyumbani mwake usiku.^b **16** Baadaye jioni hiyo, mzee fulani aliingia jijini kutoka shambani mwake. Alizaliwa katika eneo lenye milima la Efraimu,^c na kwa muda fulani alikuwa akiishi Gibea; lakini wenyeji wa jiji hilo walikuwa Wabenjamini.^d **17** Alipotazama na kumwona yule msafiri katika uwanja wa jiji, mzee huyo akamuuliza, “Unaenda wapi, na ume-toka wapi?” **18** Akajibu, “Tunatoka Bethlehemu kule Yuda nasi tunaenda mbali katika eneo lenye milima la Efraimu, nyumbani kwetu. Nilienda Bethlehemu katika nchi ya Yuda,^e nami ninaenda kwenye nyumba ya Yehova,^{*} lakini sijakaribishwa na yeyote. **19** Tuna nyasi na chakula cha kutosha kwa ajili ya punda wetu,^f na pia nina mkate^g na divai kwa ajili yangu, suria^{*} wangu, na mtumishi wangu. Hatujapungukiwa na kitu chochote.” **20** Hata hivyo, mzee huyo akasema, “Uwe na amani! Nitawapa chochote mnachohitaji. Lakini msilale hapa kwenye uwanja wa jiji.” **21** Ndipo akamkaribisha nyumbani mwake na kuwalisha^{*}

19:18 *Au labda, “ninatumikia katika nyumba ya Yehova.” **19:19, 25** *Au “mke.” **19:21** *Au “na kuwapa chakula cha mifugo.”

SURA YA 19

a Yos 18:21, 25

b Mwa 19:2

c Amu 19:1

d Yos 18:21, 28

e Amu 19:1, 2

f Mwa 24:32

g Mwa 18:5
Mwa 19:3

Safu ya 2

a Mwa 19:4, 5
Law 20:13
Ro 1:27
Iko 6:9, 10
Yud 7

b Mwa 19:6-8

c Amu 19:2

punda wake. Kisha wakanawa miguu, wakala, na kunywa.

22 Walipokuwa wakila na kunywa, wanaume fulani wahunu katika jiji hilo wakaizingira nyumba na kuugonga mlango kwa fujo, huku wakimwambia hivi mzee huyo mwenye nyumba, “Mtoe nje yule mwanamume aliyeingia nyumbani mwako, ili tufanye ngono naye.”^a **23** Ndipo mwenye nyumba akatoka nje na kuwambia, “Sivyo, ndugu zangu, msifanye uovu. Tafadhali, mtu huyu ni mgeni wangu. Msifanye jambo hili la aibu. **24** Hapa nina binti bikira na pia suria wa mwanamume huyu. Acheni niwatoe nje, ili mwatendee mambo ya aibu, ikiwa mnataka kufanya hivyo.”^b Lakini msimtendee mwanamume huyu jambo hili la aibu.”

25 Lakini wanaume hao hawakumsikiliza, basi yule mtu akamtoa nje kwa nguvu suria^{*} wake.^c Wakambaka na kumtendea vibaya usiku kucha mpaka asubuhi. Kisha kulipopambazuka wakamwacha aende zake. **26** Asubuhi na mape-ma, mwanamke huyo akaja kwenye nyumba ya yule mtu alimokuwa bwana wake, akaanguka chini mlangoni, akalala hapo mpaka kulipopambazuka. **27** Bwana wake ali-poamka asubuhi na kufungua milango ya nyumba ili atoke na kuendelea na safari, akamwona yule mwanamke, suria wake, akiwa amelala mlangoni, mikono yake ikiwa kwenye kizingiti. **28** Akamwambia, “Amka twende.” Lakini haku-sema lolote. Kwa hiyo mwana-

19:24 *Au “muwatendee vibaya kama mnavyotaka.”

mume huyo akamwinua na kumweka juu ya punda, wakaoondoka na kuelekea nyumbani.

29 Alipofika nyumbani kwake, akachukua kisu na kuikatakata ile maiti ya suria wake vipande 12, akapeleka kipande katika kila eneo* la Israeli. **30** Wote walioona jambo hilo wakasema, “Jambo kama hili halijawahi kutokea kamwe wala kuonekana tangu Waisraeli walipotoka Misri mpaaka leo. Fikirieni jambo hili,* mshauriane,^a kisha mtuambie tutakalofanya.”

20 Ndipo Waisraeli wote kutoka Dani^b hadi Beer-sheba na kutoka nchi ya Gileadi^c wakakusanyika kwa umoja* mbele za Yehova kule Mispa.^d **2** Basi wakuu wa watu na wa makabila yote ya Israeli wakachukua nafasi zao katika kutaniko la watu wa Mungu—wanajeshi 400,000 wenyewe mapanga waliotembea kwa miguu.^e

3 Wabenjamini wakasikia kwamba wanaume Waisraeli walikuwa wameenda Mispa.

Ndipo wanaume Waisraeli wakauliza, “Tuambieni, jambo hili linalochukiza lilitendekaje?”^f **4** Kwa hiyo yule Mlawi,^g mume wa mwanamke aliyeuawa, akajibu: “Mimi na suria wangu tulifika Gibea^h katika nchi ya Wabenjamini ili tulale usiku. **5** Kisha wakaaaji* wa Gibea wakaja kunishambulia na kuizingira nyumba usiku. Walitaka kuniua, lakini wakambaka suria wangu, naye akafa.ⁱ **6** Basi nikachukua maiti

19:29 *Au “kabila.” 19:30 *Tnn., “Weneni moyo wenu juu ya jambo hili.” 20:1, 8, 11 *Tnn., “kama mtu mmoja.” 20:5 *Au labda, “wamiliki wa mashamba.”

SURA YA 19
a Amu 20:7

SURA YA 20
b Yos 19:47, 48
Amu 18:29

c Yos 22:9

d 1Sa 7:5
1Sa 10:17
2Fa 25:23

e Amu 20:17
2Sa 24:9

f Amu 19:22

g Amu 19:1, 2

h Amu 19:12, 14

i Amu 19:25, 26

Safu ya 2

a Amu 19:29

b Amu 19:30

c Amu 20:18
Met 16:33

d Amu 19:22, 25

e Kum 13:5
Kum 17:7
Kum 22:22
1Ko 5:6, 13

ya suria wangu na kuikatakata vipandevipande, kisha nikavipeleka vipande hivyo katika maeneo* yote ya urithi ya Waisraeli,^a kwa sababu walitenda jambo la айбу na lenye kufedhehesha katika Israeli. **7** Sasa enyi Waisraeli wote, toeni ushauri na mapepokezo yenu^b kuhusu jambo hili.”

8 Basi watu wote waka-simama pamoja* na kusema, “Hakuna yeyote kati yetu atakayerudi katika hema lake au nyumbani kwake. **9** Hivi ndivyo tutakavyowatenda watu wa Gibea: Tuchague watu kwa kura ili waende kupigana nao.^c **10** Tutachukua wanaume 10 kati ya 100 kutoka katika makabila yote ya Israeli, na 100 kati ya 1,000 na 1,000 kati ya 10,000 wawatafutie chakula wanajeshi, ili wawadhibu wakaaaji wa Gibea katika nchi ya Benjamini, kwa sababu ya jambo hili la айбу walilotenda katika Israeli.” **11** Kwa hiyo wanaume wote Waisraeli wakakusanyika na kuungana pamoja* ili kulishambulia jiji hilo.

12 Kisha makabila ya Israeli yakatuma wanaume kwa watu wa kabila la Benjamini, wakawauliza, “Kwa nini mmetenda jambo hili linalochukiza? **13** Sasa waleteni wahuni hao wa Gibea,^d ili tuwaue na kuondoa kabisa uovu katika Israeli.”^e Lakini Wabenjamini walikataa kuwasikiliza ndugu zao Waisraeli.

14 Ndipo Wabenjamini wakakusanyika kutoka katika majiji yao kwenda Gibea ili kupigana na wanaume Waisraeli. **15** Siku hiyo Wabenjamini

20:6 *Au “makabila.”

walikusanya wanaume 26,000 wenye mapanga kutoka kati ka majiji yao, na pia wanaume 700 mashujaa kutoka Gibeaa. **16** Jeshi hilo lilikuwa na wanaume 700 mashujaa waliotumia mkono wa kushoto. Kila mmoja wao aliweza kurusha jiwe kwa kombeo na kulenga unywele* bila kukosea.

17 Waisraeli kwa upande wao walikusanya wanaume 400,000 wenye mapanga,^a na kila mmoja wao alikuwa mpiganaji mwenye uzoe fu. **18** Wakapanda kwenda Betheli kumwomba Mungu ushauri.^b Basi Waisraeli wakamuuliza hivi: “Ni nani kati yetu anayepaswa kutuongoza kupigana na Wabenjamini?” Yehova akajibu, “Kabala la Yuda litaongoza.”

19 Baada ya hayo, Waisraeli wakaamka asubuhi na kupiga kambi ili kushambulia Gibeaa.

20 Basi wanaume Waisraeli wakaenda kupigana na Wabenjamini; wakajipanga kivita ili kushambulia Gibeaa. **21** Kisha Wabenjamini wakatoka Gibeaa na kuwaua wanaume 22,000 Waisraeli siku hiyo. **22** Hata hivyo, wanajeshi Waisraeli wakaonyesha ujasiri na kujipanga tena kwa ajili ya vita mahali walipojipanga siku ya kwanza. **23** Ndipo Waisraeli wakapanda kwenda kumlilia Yehova mpaka jioni na kumuuliza hivi Yehova: “Je, twende tena kupigana na ndugu zetu, Wabenjamini?”^c Yehova akawaambia, “Pandeni mkapigane nao.”

24 Basi Waisraeli wakawakaribia Wabenjamini siku ya pili. **25** Nao Wabenjamini wakatoka Gibeaa ili kupiga-

SURA YA 20

a Amu 20:2

b Kut 28:30
Hes 27:21
Amu 20:27

c Amu 20:28

Safu ya 2

a Amu 20:21

b Amu 20:23

c 2Nya 20:3
Ezr 8:21

d Law 1:3

e Law 3:1

f Hes 27:21
Amu 20:18g Kut 6:25
Hes 25:7

h Amu 20:23

i Yos 8:3, 4

j Amu 20:20, 22

k Amu 20:36

l Amu 20:39

m Amu 20:21, 25

na nao siku ya pili, wakawaua Waisraeli wengine 18,000,^a wote wakiwa na mapanga. **26** Ndipo wanaume wote wa Israeli wakapanda kwenda Betheli. Wakalia na kukaa huko mbele za Yehova,^b nao wakafunga^c siku hiyo mpaka jioni na kumtolea Yehova dhahibu za kuteketezwa^d na dhahibu za ushirika.^e **27** Baada ya hayo, wanaume Waisraeli wakaomba ushauri wa Yehova,^f kwa kuwa sanduku la agano la Mungu wa kweli lilikuwa huko siku hizo. **28** Basi Finehasi^g mwana wa Eleazari, mwana wa Haruni, alikuwa akihudumu* mbele ya sanduku hilo siku hizo. Wakamuuliza, “Je, twende tena kupigana na ndugu zetu Wabenjamini, au tusiende?”^h Yehova akawajibu hivi: “Nendeni, kwa sababu kesho nitawatia mikononi mwenu.” **29** Ndipo Waisraeli wakaweka wanaume kuzunguka Gibeaa ili walivizie.ⁱ

30 Waisraeli wakapanda kwenda kupigana na Wabenjamini siku ya tatu, wakajipanga kivita ili kushambulia Gibeaa kama walivyofanya awali.^j **31** Wabenjamini walipoenda kupigana na jeshi hilo, walivutwa mbali na jiji.^k Kisha, kama awali, wakaanza kuwashambulia na kuwaua watu kwenye barabara kuu; barabara moja inaenda Betheli na nyingine Gibeaa, wakawaua wanaume Waisraeli wapatao 30 mashambani.^l **32** Wabenjamini wakasema, “Tunawashinda kama awali.”^m Lakini Waisraeli wakasema, “Tukimbieni na kuwavuta mbali na jiji lao waje kwenye barabara kuu.” **33** Basi wanaume

20:16 * Au “shabaha.”

20:28 * Tnn., “akisimama.”

wote wa Israeli wakatoka walipokuwa na kwenda kujipanga kivita kule Baal-tamari, na Waisraeli waliokuwa wakivizia wakatoka mahali walipokuwa wamejificha karibu na Gibeaa. **34** Kisha wanaume 10,000 mashujaa kutoka kotekote Israeli wakaja mbele ya Gibeaa, na mapigano yakawa makali. Lakini Wabenjamini hawakujua kwamba walikuwa karibu kuangamizwa.

35 Yehova akawashinda Wabenjamini^a mbele ya Waisraeli; siku hiyo Waisraeli waliwaua wanaume 25,100 Wabenjamini waliokuwa na mapanga.^b

36 Hata hivyo, wanaume Waisraeli walipokimbia kutoka Benjamini,^c Wabenjamini walifikiri kwamba wangewashinda, lakini walikimbia kwa sababu waliwategemea Waisraeli wenzao waliokuwa wakivizia jiji la Gibeaa.^d **37** Na wale waliokuwa wakivizia wakatokea haraka na kukimbia kuelekea Gibeaa. Wakasambaa na kuwaua kwa upanga watu wote waliokuwa jijini.

38 Basi wanaume wa Israeli walikuwa wamepanga kwamba wanaume waliovizia jiji watoe ishara kwa kufanya moshi upande juu kutoka jijini.

39 Waisraeli walipogeuka na kukimbia, wanaume Wabenjamini wakaanza kuwashambulia, wakawaua wanaume Waisraeli wapatao 30,^e huku wakisema, "Ni wazi kwamba tunawashinda tena, kama tulivyowashinda awali."^f **40** Lakini ile ishara ya wingu la moshi ikaanza kupanda kutoka jijini. Wabenjamini walipogeuka, waliona moto ukitekeza jiji lote na moshi ukipanda angani. **41** Kisha wanaume

SURA YA 20

a Amu 20:28, 48

b Amu 20:14, 15
Amu 20:46

c Amu 20:31

d Amu 20:29

e Amu 20:31

f Amu 20:21, 25

Safu ya 2

a Amu 20:15

b Amu 21:13

c Amu 20:15, 35

SURA YA 21

d Amu 20:1

e Amu 21:18

Waisraeli wakageuka kwa ghafila na kuwakimbiza, Wabenjamini wakashtuka, kwa kuwa waliona kwamba wataangamizwa. **42** Basi wakawakimbia wanaume Waisraeli na kuelekea nyikani, lakini Waisraeli wakawakimbiza na kuwashambulia; wanaume Waisraeli waliotoka majijini wakawashambulia pia na kuwaua. **43** Wakawazingira Wabenjamini na kuwafuata himahima. Wakawakanyaga-kanyaga mbele ya Gibeaa, upande wa mashariki. **44** Hatimaye wanaume 18,000 Wabenjamini wakaangamizwa, wote walikuwa mashujaa hodari.^a

45 Basi wanaume Wabenjamini wakageuka na kukimbilia nyikani kwenye mwamba wa Rimoni,^b na Waisraeli wakawaua Wabenjamini 5,000 kwenye barabara kuu, nao wakaendelea kuwafuatia mpaka Gidomu; wakawaua wanaume wengine 2,000. **46** Siku hiyo, Wabenjamini 25,000 wenyewe mapanga waliuaua,^c wote walikuwa mashujaa hodari. **47** Lakini wanaume 600 walikimbilia nyikani kwenye mwamba wa Rimoni, na kuka kwenye mwamba huo kwa miezi minne.

48 Na wanaume Waisraeli wakarudi kuwashambulia Wabenjamini na kuwaua kwa upanga watu wote waliokuwa jijini pamoja na mifugo, kila kitu kilichobaki. Pia, walitekeza kwa moto majiji yote katika maeneo waliyopitia.

21 Sasa wanaume Waisraeli walikuwa wameapa hivi kule Mispaa:^d "Hakuna yeyote kati yetu atakayekubali binti yake aolewe na mwanaume Mbenjamini."^e **2** Kwa

hiyo, watu wakaja Betheli^a na kukaa huko mbele za Mungu wa kweli mpaka jioni, wakipaza sauti na kulia kwa uchungu. **3** Nao walikuwa wakisema hivi: “Ee Yehova Mungu wa Israeli, kwa nini jambo hili limetokea katika Israeli? Kwa nini tukose kabila moja la Israeli leo?” **4** Siku iliyofuata, watu wakaamka mapema na kujenga madhabahu hapo ili watoe dhahibu za kuteketezwa na dhahibu za ushirika.^b

5 Kisha Waisraeli wakaulizana, “Ni kabila gani kati ya makabila yote ya Israeli ambalo halikukusanyika mbele za Yehova?”^c kwa kuwa walifanya kiapo kikubwa kwamba yeyote ambaye hakufika Mispā mbele za Yehova lazima auawe. **6** Basi Waisraeli wakahuzunika kwa sababu ya mambo yaliyowapata ndugu zao Wabenjamini. Wakasema, “Leo kabila moja limekatwa kutoka Israeli. **7** Kwa kuwa tumeapa mbele za Yehova^c kwamba hatutakubali kamwe binti zetu waolewe nao, tutapata wapi wake kwa ajili ya wanaume waliobaki?”^d

8 Wakaulizana, “Ni kabila gani la Israeli ambalo halikufika Mispā mbele za Yehova?”^e Wakagundua kwamba hakuna yeyote kutoka Yabesh-gileadi aliyekuja kambini kukusanyika na Waisraeli wengine. **9** Watu walipohesabiwa, wakagundua kwamba hakuna mkaaji hata mmoja wa Yabesh-gileadi aliyekuwepo. **10** Basi wakawatuma wanau-me 12,000 waliokuwa mashujaa zaidi. Wakawaamuru hivi: “Nendeni, mkawaue kwa upanga wakaaji wa Yabesh-gileadi, msiache wanawake wala wa-

SURA YA 21

a Amu 20:18, 26

b Law 3:1

c Law 5:4
Law 19:12
Mt 5:33

d Amu 21:1, 18

e Amu 20:1

Safu ya 2

a Amu 21:5

b Yos 18:1

c Amu 20:46, 47

d Amu 21:8, 12

e Amu 21:6

f Law 19:12
Amu 21:1

g Yos 18:1

toto.^a **11** Hivi ndivyo mnavyopaswa kufanya: mnapaswa kumwangamiza kila mwanamume, na pia kila mwanamke ambaye amefanya ngono na mwanamume.” **12** Miongoni mwa wakaaji wa Yabesh-gileadi walipata mabikira 400 ambao hawajawahi kufanya ngono na mwanamume. Basi wakawaleta kambini huko Shilo,^b katika nchi ya Kanaani.

13 Kisha Waisraeli waliokusanyika wakawatumia ujumbe wa amani Wabenjamini waliokuwa kwenye mwamba wa Rimoni.^c **14** Basi Wabenjamini wakarudi wakati huo. Waisraeli wakawapa Wabenjamini wanawake waliowachukua kule Yabesh-gileadi,^d lakini walikuwa wachache kuliko wanaume. **15** Na watu wakahuzunika kwa sababu ya mambo yaliyowapata Wabenjamini^e kwa kuwa Yehova alileta mgawanyiko katika makabila ya Israeli. **16** Wazee wa Waisraeli wakauliza, “Kwa kuwa wanawake wote Wabenjamini waliuawa, tufanye nini ili tupate wake kwa ajili ya wanau-me waliobaki?” **17** Wakajibu, “Wabenjamini waliobaki wanaswa kupewa urithi ili kabila lolote lisiangamizwe kutoka Israeli. **18** Lakini haturuhusiwi kuwapa binti zetu wawe wake zao, kwa sababu Waisraeli wameapa hivi: ‘Alaaniwe yeyote anayempa Mbenjamini mke.’”^f

19 Ndipo wakasema, “Jamani! Kuna sherehe ya Yehova inayofanywa kila mwaka kule Shilo,^g jiji lililo upande wa kaskazini wa Betheli na upande wa mashariki wa barabara kuu inayopanda kutoka Betheli kwenda Shekemu

na upande wa kusini wa Lebona.” **20** Kisha wakawaamuru hivi wanaume Wabenjamini: “Nendeni mkavizie katika mashamba ya mizabibu. **21** Mta- kapoona wasichana wa* Shilo wakitoka ili kucheza dansi za mzunguko, tokeni katika mashamba ya mizabibu na kila mmoja wenu ajichukulie mke miongoni mwa wasichana hao wa Shilo, kisha mrudi katika nchi ya Benjamini. **22** Na baba zao au ndugu zao wakija kutulalamikia, tutawaambia, “Tutendeeni kwa fadhili kwa niaba yao, kwa sababu tulipoenda vitani hatukuweza kupata mke kwa ajili ya kila mmoja wao,^a nanyi hamngewe-

21:21 *Tnn., “mabinti wa.”

SURA YA 21
a Amu 21:12, 14

Safu ya 2
a Amu 21:1, 18

b Amu 20:48

c Amu 17:6
1Sa 8:4, 5

za kuwapa wake na kuepuka hatia.”^a

23 Basi hivyo ndivyo wanaume Wabenjamini wali- vyofanya; walijichukulia wake miongoni mwa wanawake waliokuwa wakicheza dansi. Kisha wakarudi katika urithi wao, wakajenga tena majiji yao,^b na kuishi humo.

24 Wakati huo Waisraeli wakatawanyika kutoka huko, na kila mmoja akarudi kwa kabila lake na kwa ukoo wake, kila mmoja akarudi katika urithi wake.

25 Siku hizo hakukuwa na mfalme katika Israeli.^c Kila mtu alifanya jambo aliloona ni jema machoni pake.*

21:25 *Au “alilofikiri linafaa.”

RUTHU

YALIYOMO

- Elimeleki na familia yake wahamia Moabu (1, 2)
Naomi, Orpa, na Ruthu wafiwa na waume zao (3-6)
Ruthu aonyesha ushikamanifu kwa Naomi na kwa Mungu wa Naomi (7-17)
Naomi arudi Bethlehemu pamoja na Ruthu (18-22)
- Ruthu aokota masuke ya nafaka katika shamba la Boazi (1-3)

- Ruthu na Boazi wakutana (4-16)
Ruthu amweleza Naomi kuhusu fadhili za Boazi (17-23)
- Naomi ampa Ruthu maagizo (1-4)
Ruthu na Boazi kwenye uwanja wa kupuria nafaka (5-15)
Ruthu arudi kwa Naomi (16-18)
- Boazi awa mkombozi (1-12)
Boazi na Ruthu wamzaa Obedi (13-17)
Ukoo wa Daudi (18-22)

1 Basi katika siku ambazo waamuzi^a walikuwa waki- tekeleza hukumu,* kulikuwa na njaa kali nchini; na mwanamume fulani akatoka Beth-

1:1 *Tnn., “wakihukumu.”

SURA YA 1
a Amu 2:16

Safu ya 2
a Mik 5:2
b Mwa 19:36, 37
Kum 2:9
Amu 3:30

lehemu^a huko Yuda akahamia katika mashamba ya* Moabu akiwa mgeni,^b yeye, pamoja na mke wake, na watoto wake wawili wa kiume.

1:1 *Au “eneo la.”

2 Mwanamume huyo aliitwa Elimeleki,* na mke wake alii-twa Naomi,# na watoto wake wawili waliitwa Maloni^Δ na Kili-^Ωlioni.^Ω Walikuwa Waefrathi kutoka Bethlehemu nchini Yuda. Wakafika katika mashamba ya Moabu na kuishi huko.

3 Baada ya muda, Elimeleki mume wa Naomi akafa, naye akabaki na wanawe wawili.

4 Baadaye wana hao wakaoa wanawake Wamoabu; mmoja aliitwa Orpa, na mwingine alii-twa Ruthu.^a Waliishi huko kwa miaka kumi hivi. **5** Kisha wana hao wawili, Maloni na Kili-^Ωlioni wakafa pia, Naomi akabaki bila watoto wake wawili na bila mume wake. **6** Akaanza safari kutoka katika mashamba ya Moabu pamoja na binti wakwe zake, kwa maana akiwa Moabu alisikia kwamba Yehova alikuwa amewalekezea uangalifu watu Wake kwa kuwapa chakula.*

7 Akaondoka mahali alipo-kuwa akiishi pamoja na binti wakwe zake wawili. Walipokuwa wakitembea njiani kurudi katika nchi ya Yuda, **8** Naomi akawaambia: “Nendeni, rudini kila mmoja wenu nyumbani kwa mama yake. Yehova na awatendee kwa upendo mshikamanifu,^b kama tu mliyowatandea waume zenu ambao wamekufa na kama mliyvitendea mimi. **9** Yehova na awabariki* ili kila mmoja wenu apate usalama# kati-

1:2 *Maana yake “Mungu Wangu Ni Mfalme.” #Maana yake “Uzuri Wangu.”

^ΔLabda linatokana na neno la Kiebrania linalomaanisha “kuwa dhaifu; kuwa mgonjwa.” ^ΩMaana yake “Anayeshindwa; Anayefikia Mwisho.” 1:6 *Tnn., “mkate.” 1:9 *Tnn., “awape zawadi.” #Tnn., “apate mahali pa kupumzika.”

SURA YA 1

a Mt 1:5

b Kut 34:6
Ru 2:20

Safu ya 2

a Ru 3:1

b Kum 25:5,6

c Ru 1:20

d Ru 2:11,12

ka nyumba ya mume wake.”^a Kisha akawabusu, nao wakalia kwa sauti kubwa. **10** Wakamwambia tena na tena: “Hapana, tutaenda nawe kwa watu wako.” **11** Lakini Naomi akawaambia: “Rudini binti zangu. Kwa nini mnifuate? Je, ninaweza tena kuzaa watoto ambao watakuwa waume zenu?”^b **12** Rudini, binti zangu. Nendeni, kwa maana nimezeeka sana siwezi kuolewa tena. Hata kama ningetumaini kupata mume usiku wa leo na kuzaa watoto pia, **13** je, mngeendelea kuwangojea ili wakue? Je, mgekataa kuolewa tena mkiwasubiri? Hapana, binti zangu, nina chungu mwingi kwa ajili yenu, kwa sababu mkono wa Yehova umegeuka dhidi yangu.”^c

14 Wakalia tena kwa sauti kubwa, kisha Orpa akambusu mama mkwe wake na kwenda zake. Lakini Ruthu akashikamana naye. **15** Kwa hiyo Naomi akamwambia: “Tazama! Dada mkwe mwenzako mjane amerudi kwa watu wake na kwa miungu yake. Rudi pamoja na dada mkwe mwenzako.”

16 Lakini Ruthu akasema: “Usinisihi nikuache, nirudi na kuacha kukufuata; kwa maana mahali utakapoenda nitaenda, na mahali utakapolala usiku hapo ndipo nitakapolala pia. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu.”^d

17 Mahali utakapokufa nita-fia hapo, na hapo ndipo nitakapozikwa. Yehova na ania-dhibu, tena vikali, ikiwa kitu chochote kitanitenganisha nawe isipokuwa kifo.”

18 Naomi alipoona kwamba Ruthu anasisitiza kwe-

nda naye, hakuendelea kumshihi asimfuate. **19** Wote wawili wakaendelea na safari mpaka walipofika Bethlehemu.^a Mara tu walipofika Bethlehemu, jiji lote likasisimka kwa sababu yao, na wanawake wakaulizana: “Je, huyu ni Naomi?” **20** Naye aliwambia: “Msiniite Naomi.* Niite ni Mara,[#] kwa maana Mweza-Yote amefanya maisha yawe machungu sana kwangu.^b **21** Mikono yangu ilikuwa imejaa nilipoenda, lakini Yehova amenifanya nirudi mikono mitupu. Kwa nini mniite Naomi, wakati Yehova ndiye aliyenipinga na Mweza-Yote ndiye aliyeniletea msiba?”^c

22 Hivyo ndivyo Naomi alivyorudi kutoka katika mashamba ya Moabu^d pamoja na Ruthu, binti mkwe wake Mmoabu. Walifika Bethlehemu mwanzoni mwa mavuno ya shayiri.^e

2 Basi Naomi alikuwa na mtu wa ukoo wa Elimeleki, mume wake; mtu huyo aliitwa Boazi^f na alikuwa tajiri sana.

2 Ruthu Mmoabu akamwambia Naomi: “Tafadhali, niruhusu niende mashambani nikaokote masalio^g ya masuke ya nafaka nyuma ya yeyote yule atakayeniruhusu.” Basi Naomi akamwambia: “Nenda, binti yangu.” **3** Basi akaenda na kuanza kuokota masalio mashambani nyuma ya wavunaji. Bila kutarajia akajikuta katika shamba la Boazi,^h aliyekuwa wa ukoo wa Elimeleki.ⁱ **4** Ndipo Boazi akaja kutoka Bethlehemu na kuwambia wavunaji: “Yehova na

1:20 *Maana yake “Uzuri Wangu.”
#Maana yake “Uchungu.”

SURA YA 1

a Ru 1:1, 2

b Ru 1:13

c Ru 1:3, 5

d Hes 21:13
Ru 1:1

e Ru 2:23

SURA YA 2

f Ru 2:20
Ru 4:21, 22
Mt 1:5
Lu 3:23, 32g Law 23:22
Kum 24:19

h Ru 2:20

i Ru 1:2

Safu ya 2

a Ru 1:3, 4

b Ru 1:16, 22

c Law 23:22
Kum 24:19

d Ru 2:22

e Kut 23:9
Law 19:34

f Ru 1:14, 16

g Ru 4:11, 17
Mt 1:5, 16

awe pamoja nanyi.” Nao waka-jibu: “Yehova na akubariki.”

5 Kisha Boazi akamuuliza kijana aliyekuwa msimamizi wa wavunaji: “Msichana huyu ni wa nani?” **6** Kijana aliyekuwa msimamizi wa wavunaji akamjibu: “Msichana huyu ni Mmoabu,^a aliyerudi na Naomi kutoka katika mashamba ya Moabu.^b **7** Aliniuliza, “Tafadhali, ninaweza kuokota^c na kukusanya masuke* ya nafaka yaliyoachwa na wavunaji?” Amekuwa akifanya kazi tangu alipokuja asubuhi, ni sasa tu ameketi kibandani ili kupumzika kidogo.”

8 Kisha Boazi akamwambia Ruthu: “Sikiliza, binti yangu. Usiende kuokota masalio katika shamba lingine, wala usiende mahali pengine popote; uwe karibu na wafanyakazi wangu wasichana.^d **9** Angalia shamba wanalovuna, nawe uwafuate. Nimewaamuru wale vijana wa kiume wasikuguse.* Ukihisi kiu, nenda kwenye mitungi ya maji ukanywe maji yaliyotekwa na hao vijana.”

10 Ndipo Ruthu akapiga magoti na kuinama mpaka chini na kumwambia: “Nimepataje kibali machoni pako, na kwa nini umenijali ilhali mimi ni mgeni?”^e **11** Boazi akamjibu: “Nimeambiwa mambo yote uliyomfanyia mama mkwe wako baada ya mume wako kufa na jinsi ulivyomwacha baba yako na mama yako na nchi ya watu wako wa ukoo ukaja kwa watu ambao hukuwajua.^f **12** Yehova na akuthawabishe kwa yale uliyofanya,^g na upate malipo* kamili kutoka kwa

2:7 *Au labda, “matita.” 2:9 *Au “wasikusumbue.” 2:12 *Au “thawabu.”

Yehova Mungu wa Israeli, ambaye umekuja kutafuta kimbilio chini ya mabawa yake.”^a

13 Basi Ruthu akasema: “Acha nipate kibali machoni pako, bwana wangu, kwa sababu umenifariji na kunitia moyo,* ingawa mimi hata si mmoja wa watumishi wako.”

14 Wakati wa chakula, Boazi akamwambia: “Njoo hapa, ule mkate na kuuchovya katika siki.” Basi Ruthu akaketi kando ya wavunaji. Boazi akampa nafaka zilizokaangwa, akala, akashiba, na kubakiza. **15** Aliposimama ili aokote masuke ya nafaka,^b Boazi akawaamuru hivi watumishi wake: “Mwacheni aokote masuke* ya nafaka yaliyokatawa pia, msimtese.^c **16** Pia, hakikisheni kwamba mnachomoa masuke machache kutoka katika matita na kumwachia nyuma ili ayaokote, msimkataze.”

17 Basi akaendelea kuokota masuke shambani mpaka jioni.^d Alipoyapura, alipata karibu efa* moja ya shayiri. **18** Halafu akachukua nafaka hiyo na kwenda jijini, na mama mkwe wake akaoa nafaka aliyokuwa ameokota. Halafu Ruthu akachukua chakula alichokuwa amebakiza^e baada ya kula na kushiba, akampa.

19 Basi mama mkwe wake akamuuliza: “Leo uliokota masuke wapi? Ulifanya kazi wapi? Na abarikiwe yule aliyekute ndea kwa fadhili.”^f Ndipo akamwambia mama mkwe wake

2:13 *Tnn., “umezungumza na moyo wangu.” 2:15 *Au labda, “matita.” 2:17 *Karibu kilogramu 13. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 2

a Zb 17:8
Zb 36:7
Zb 57:1
Zb 63:7

b Law 19:9
Ru 2:2

c Ru 2:9

d Ru 2:7

e Ru 2:14

f Zb 41:1

Safu ya 2

a Kut 34:6
Ru 1:8
Zb 36:7

b Ru 2:1

c Law 25:25
Kum 25:5, 6
Ru 3:9, 12

d Ru 2:8

e Ru 1:22

f Ru 1:16

SURA YA 3

g Ru 1:9

h Ru 2:1, 20

kuhusu mtu aliyefanya kazi katika shamba lake: “Nilifanya kazi katika shamba la mwanamume anayeitwa Boazi.”

20 Basi Naomi akamwambia binti mkwe wake: “Na abarikiwe na Yehova, ambaye hajawahi kamwe kukosa kuwatendea kwa upendo mshikamanifu walio hai na walio kufa.”^a Naomi akaendelea kusema: “Mwanamume huyo ni mtu wetu wa ukoo.^b Yeye ni kati ya watu wanaoweza kutukomboa.”^{*c} **21** Ndipo Ruthu Mmoabu akasema: “Pia aliniambia, ‘Uwe karibu na watumishi wangu mpaka watakapomaliza kuvuna mavuno yangu yote.’”^d **22** Naomi akamwambia Ruthu binti mkwe wake: “Binti yangu, ni afadhali ufuatane na wafanyakazi wake wasichana, usije ukasumbuliwa katika shamba lingine.”

23 Kwa hiyo akafuatana na wasichana wa Boazi na kuokota masuke mpaka mwisho wa mavuno ya shayiri^e na mavuno ya ngano. Naye akaendelea kuishi na mama mkwe wake.^f

3 Basi Naomi mama mkwe wake akamwambia: “Binti yangu, je, si vema nikutafutie makao*^g ili mambo yakunde vyema? **2** Boazi, ambaye ulifanya kazi na wasichana wake, je, yeye si mtu wetu wa ukoo?^h Usiku wa leo anapepete shayiri kwenye uwanja wa kupuria. **3** Basi oga na ujipake mafuta yenye marashi; kisha uvae vizuri na kwenda kwenye uwanja wa kupuria. Hakikisha hakuoni hadi atakapomaliza kula na kunywa.

2:20 *Au “mmojawapo wa watu wetu wa ukoo walio na haki ya kutukomboa.” 3:1 *Tnn., “mahali pa kumpumzika.”

4 Atakapolala, angalia mahali ambapo atalala; kisha uende ufunue miguu yake na ulale hapo. Atakwambia jambo unalopaswa kufanya.”

5 Basi Ruthu akasema: “Yote unayoniambia nitafanya.”

6 Kwa hiyo, akaenda kwenye uwanja wa kupuria na kufanya yote aliyoambiwa na mama mkwe wake.

7 Basi Boazi akala, akanywa, na kuchangamka moyoni. Kisha akaenda kulala mwisho wa rundo la nafaka. Kisha Ruthu akaja kimyakimya, akamfunua miguu, na kulala hapo.

8 Katikati ya usiku, mwanamume huyo alianza kutetemeka, akaketi na kumwona mwanamke amelala miguuni pake.

9 Akamuuliza: “Wewe ni nani?” Akajibu: “Mimi ni Ruthu, kijakazi wako. Nifunike mimi kijakazi wako kwa vazi lako,*

kwa maana wewe ni mkombozi.”^a

10 Basi Boazi akasema: “Yehova na akubariki, binti yangu. Wakati huu, umetenda kwa upendo mshikamanifu zaidi kuliko mwanzoni,^b kwa kuwa hukuwafuata wale vijana, matajiri au maskini.

11 Na sasa binti yangu, usiogope. Nitakufanyia kila jambo utakalosema,^c kwa maana kila mtu jijini* anajua kwamba wewe ni mwanamke bora.

12 Ni kweli kwamba mimi ni mkombozi,^d lakini kuna mkombozi ambaye ni mtu wa karibu zaidi wa ukoo kuliko mimi.^e

13 Kaa hapa usiku wa leo, na ikiwa atakukomboa asubuhi, ni sawa! Na akukomboa.^f Laki-

3:9 *Au “pindo la vazi lako.” 3:11 *Tnn., “katika lango lote la watu wangu.”

SURA YA 3

a Law 25:25
Kum 25:5, 6
Ru 2:20

b Ru 1:14, 16

c Ru 3:9

d Law 25:25
Ru 2:20

e Ru 4:1

f Ru 4:5

Safu ya 2

SURA YA 4

a Kum 25:7
Met 31:23

b Ru 3:12

c Kum 16:18

ni ikiwa hataki kukukomboa, kwa hakika kama Yehova anavyoishi, mimi mwenyewe nita-kukomboa. Lala hapa mpaka asubuhi.”

14 Basi akalala miguuni pake mpaka asubuhi, kisha akaamka kabla ya mapambazuko wakati ambapo ni vigumu kumtambua yeyote. Boazi akasema: “Isijulikane kwamba mwanamke alikuja kwenye uwanja wa kupuria.”

15 Naye akaendelea kusema: “Kilete kitambaa ulichojifunika ukitandaze.” Basi Ruthu akakitandaza, naye Boazi akampimia vipimo sita* vya shayiri na kumtwika, kisha Boazi akaenda jijini.

16 Ruthu akaenda kwa mama mkwe wake, ambaye alimuuliza: “Mambo yalielendaje,* binti yangu?” Akamwambia yote ambayo mwanamume huyo alimtenda.

17 Tena akasema: “Alinipa vipimo hivi sita vya shayiri na kuniambia, ‘Usiende kwa mama mkwe wako mikono mitupu.’”

18 Basi Naomi akamwambia: “Kaa hapa binti yangu, mpaka utakapojua jinsi itakavyokuwa, kwa maana mwanamume huyo hatapumzika mpaka atakapotimiza jambo hilo leo.”

4 Sasa Boazi akapanda kwenenda kwenye lango la jiji^a na kuketi hapo. Na tazama! yule mkombozi ambaye Boazi alimtaja^b alikuwa akipita. Basi Boazi akanwita: “Fulani wa fulani, njoo, keti hapa.” Akaja na kuketi. 2 Kisha Boazi akawaita wazee kumi wa jiji,^c

3:15 *Labda vipimo sita vya sea, au karibu kilogramu 20. Angalia Nyongeza B14. 3:16 *Tnn., “Wewe ni nani?”

akawaambia: “Ketini hapa.” Nao wakaketi.

3 Ndipo Boazi akamwambia mkombozi huyo:^a “Naomi aliyerudi kutoka katika mashamba ya Moabu^b hana budi kuza shamba la ndugu yetu Elimeleki.^c **4** Niliona niku-fahamishe jambo hilo na ku-kwambia, ‘Linunue mbele ya wakaaji na wazee wa watu wangu.^d Ikiwa utalikomboa, likomboe. Lakini ikiwa hutalikomboa, niambie ili nijue, kwa maana una haki ya kulikomboa, mimi ni wa pili.’” Mtu huyo akasema: “Niko tayari kulikomboa.”^e **5** Kisha Boazi akamwambia: “Siku utakapolinunua shamba hilo kutoka kwa Naomi, unapaswa kulinunua pia kutoka kwa Ruthu Mmoabu, mke wa mwanamume aliyekufa, ili kurudisha jina la mume wake aliyekufa katika urithi huo.”^f **6** Basi mkombozi huyo akasema: “Siwezi kulikomboa kwa maana huenda nikaharibu urithi wangu mwenyewe. Likomboe kwa ajili yako mwenyewe ukitumia haki yangu ya kuko-mboa, kwa sababu siwezi kulikomboa.”

7 Ili kihalalisha makubaliano yoyote, hii ndiyo desturi iliyofuatwa zamani katika Israeli kuhusu haki ya kukomboa na kubadilishana vitu: Mtu alipaswa kuvua kiatu chake^g na kumpa mwenzake, na huo ndio utaratibu uliofuatwa ili kuthibitisha* makubaliano katika Israeli. **8** Kwa hiyo mkombozi huyo alivua kiatu alipomwambia Boazi, “Linunue liwe lako.” **9** Kisha Boazi akawaambia wazee na

4:7 *Au “kutoa ushuhuda wa.”

SURA YA 4

a Law 25:25
Kum 25:5, 6
Ru 2:20
Ru 3:9, 12

b Ru 1:1, 6

c Ru 1:2

d Mwa 23:18
Yer 32:9, 10

e Ru 3:13

f Mwa 38:7, 8
Kum 25:5, 6

g Kum 25:7, 9

Safu ya 2

a Mwa 23:18
Ru 4:4
Yer 32:12

b Mwa 38:7, 8
Kum 25:5, 6

c Ru 4:4

d Mwa 28:3
Mwa 35:23-26
Mwa 46:15, 18
Mwa 46:22, 25

e Mwa 35:19

f Ru 1:1
Mik 5:2

g Mwa 38:29
Hes 26:20
Mt 1:3

h Zb 127:3

i Ru 1:14, 16

watu wote waliokuwepo: “Ninyi ni mashahidi^a leo kwamba ninanunua kutoka kwa Naomi vitu vyote vilivyokuwa vya Elimeleki na vitu vyote vilivyokuwa vya Kilioni na Maloni. **10** Namchukua pia Ruthu Mmoabu, mke wa Maloni, awe mke wangu ili kurudisha jina la mwanamume huyo aliyekufa katika urithi wake,^b ili jina la mwanamume huyo aliyekufa lisifutiliwe mbali kutoka kati ya ndugu zake na kutoka katika lango la jiji lake. Ninyi ni mashahidi leo.”^c

11 Ndipo watu wote waliokuwa katika lango la jiji na wale wazee wakasema: “Sisi ni mashahidi! Yehova na ambariki mke anayekuja nyumbani mwako ili awe kama Raheli na Lea, ambao walijenga nyumba ya Israeli.^d Ufanikiwe katika Efratha^e na ujijengee jina zuri* katika Bethlehemu.^f **12** Nyumba yako na iwe kama nyumba ya Perezi,^g ambaye Tamari alimzalia Yuda, kupitia uzao ambao Yehova atakupa kutoka kwa mwanamke huyu kijana.”^h

13 Basi Boazi akamwoa Ruthu. Akalala naye, na Yehova akamwezesha kupata mimba na kuzaa mwana.

14 Halafu wanawake wakamwambia Naomi: “Yehova na asifiwe, ambaye hakukuacha bila mkombozi leo. Jina la mwana huyo na litangazwe katika Israeli!

15 Yeye* amekurudishia uhai wako[#] na atakutunza uzee-ni, kwa sababu amezaliwa na binti mkwe wako anayekupenda’ na ambaye ni bora kwako

4:11 *Tnn., “utangaze jina.” 4:15 *Yaa-ni, mjukuu wa Naomi. #Au “nafsi yako.”

kuliko wana saba.” **16** Naomi akamchukua mtoto huyo na kumbeba kifuani, naye akamtunza.* **17** Kisha wana wake majirani wakampa jina. Wakasema, “Naomi amezaa mwana,” nao wakamwita Obedi.^a Yeye ndiye baba ya Yese,^b aliyemzaa Daudi.

18 Basi huu ndio ukoo

4:16 *Au “akawa mlezi wake.”

SURA YA 4

a Mt 1:5
Lu 3:23, 32
b 1Sa 17:12
Isa 11:1
Ro 15:12

Safu ya 2

a Ru 4:12
Mt 1:2-6
b Mwa 46:12
Hes 26:21
1Nya 2:5
c 1Nya 2:9-15
d Kut 6:23
e Ru 4:17
1Sa 16:1
f 2Sa 7:8
1Nya 2:13, 15

wa* Perezi;^a Perezi alimzaa Hezroni;^b **19** Hezroni akamzaa Ramu; Ramu akamzaa Aminadabu;^c **20** Aminadabu^d akamzaa Nashoni; Nashoni akamzaa Salmoni; **21** Salmoni akamzaa Boazi; Boazi akamzaa Obedi; **22** Obedi akamzaa Yese;^e na Yese akamzaa Daudi.^f

4:18 *Tnn., “hivi ndivyo vizazi vya.”

KITABU CHA KWANZA CHA

SAMWELI

YALIYOMO

- | | |
|--|---|
| <p>1 Elkana na wake zake (1-8)
Hana ambaye hakuwa na mtoto asali apate mwana (9-18)
Samweli azaliwa na kukabidhiwa kwa Yehova (19-28)</p> <p>2 Sala ya Hana (1-11)
Dhambi za wana wawili wa Eli (12-26)
Yehova aihukumu nyumba ya Eli (27-36)</p> <p>3 Samweli aitwa awe nabii (1-21)</p> <p>4 Wafilisti wateka sanduku la agano (1-11)
Eli na wanawe wafa (12-22)</p> <p>5 Sanduku la agano katika eneo la Wafilisti (1-12)
Dagoni aaibishwa (1-5)
Wafilisti waletewa pigo (6-12)</p> <p>6 Wafilisti warudisha sanduku la agano Israeli (1-21)</p> <p>7 Sanduku la agano laletwa Kiriath-yearimu (1)
Samweli ahimiza hivi: ‘Mtumikieni Yehova peke yake’ (2-6)
Ushindi wa Waisraeli kule Mispa (7-14)
Samweli awa mwamuzi wa Israeli (15-17)</p> <p>8 Waisraeli wataka mfalme (1-9)
Samweli awaonya watu (10-18)
Yehova akubali ombi la kutaka mfalme (19-22)</p> | <p>9 Samweli akutana na Sauli (1-27)</p> <p>10 Sauli atiwa mafuta kuwa mfalme (1-16)
Sauli atangazwa kuwa mfalme mbeke ya watu (17-27)</p> <p>11 Sauli awashinda Waamoni (1-11)
Sauli atangazwa tena kuwa mfalme (12-15)</p> <p>12 Hotuba ya mwisho ya Samweli (1-25)
‘Msifuata vitu vya ubatili’ (21)
Yehova hatawaacha watu wake (22)</p> <p>13 Sauli achagua jeshi (1-4)
Sauli atenda kwa kimbelembele (5-9)
Samweli amkaripia Sauli (10-14)
Waisraeli hawakuwa na silaha (15-23)</p> <p>14 Yonathani aenda kupigana kule Mikmashi (1-14)
Mungu awashinda maadui wa Waisraeli (15-23)
Sauli afanya kiapo bila kufikiria (24-46)
Watu wala nyama pamoja na damu (32-34)
Vita vya Sauli; familia yake (47-52)</p> <p>15 Sauli akosa kutii kwa kumwacha hai Agagi (1-9)
Samweli amkaripia Sauli (10-23)
“Kutii ni bora kuliko dhabihu” (22)</p> |
|--|---|

- Sauli akataliwa asiendelee kuwa mfalme (24-29)
Samweli amuua Agagi (30-35)
- 16 Samweli amtia mafuta Daudi kuwa mfalme anayefuata (1-13)
"Yehova huona ndani ya moyo" (7)
Sauli anyang'anywa roho ya Mungu (14-17)
Daudi awa mpiga kinubi wa Sauli (18-23)
- 17 Daudi amshinda Goliathi (1-58)
Goliathi awatukana Waisraeli (8-10)
Daudi akubali kupigana na Goliathi (32-37)
Daudi apigana kwa jina la Yehova (45-47)
- 18 Urafiki wa Daudi na Yonathani (1-4)
Sauli ashikwa na wivu kwa sababu ya ushindi wa Daudi (5-9)
Sauli ajaribu kumuua Daudi (10-19)
Daudi amwoa Mikali binti ya Sauli (20-30)
- 19 Sauli aendelea kumchukia Daudi (1-13)
Daudi amkimbia Sauli (14-24)
- 20 Yonathani awa mshikamanifu kwa Daudi (1-42)
- 21 Daudi ala mikate ya wonyesho kule Nobu (1-9)
Daudi ajifanya mwenda wazimu kule Gathi (10-15)
- 22 Daudi akiwa Adulamu na Mispe (1-5)
Sauli aagiza makuhani wa Nobu wauawe (6-19)
Abiathari atoroka (20-23)
- 23 Daudi aliokoa jiji la Keila (1-12)
Sauli amfuatia Daudi (13-15)
Yonathani amtia nguvu Daudi (16-18)
Daudi anusurika kukamatwa na Sauli (19-29)
- 24 Daudi amwacha hai Sauli (1-22)
Daudi amheshimu mtiwa-mafuta wa Yehova (6)
- 25 Kifo cha Samweli (1)
Nabali awafukuza wanaume wa Daudi (2-13)
Abigaili atenda kwa hekima (14-35)
'Yehova ataufungia uhai katika mfuko wa uzima' (29)
Yehova amuua Nabali aliyekuwa mpumbavu (36-38)
Abigaili awa mke wa Daudi (39-44)
- 26 Daudi amwacha hai tena Sauli (1-25)
Daudi amheshimu mtiwa-mafuta wa Yehova (11)
- 27 Wafilisti wampa Daudi Siklagi (1-12)
- 28 Sauli amtembelea mtu anayewasiliana na roho waovu kule En-dori (1-25)
- 29 Wafilisti hawamwamini Daudi (1-11)
- 30 Waamaleki wavamia na kuchoma moto Siklagi (1-6)
Daudi apata nguvu kutoka kwa Mungu (6)
Daudi awashinda Waamaleki (7-31)
Watu waliotekwa wachukuliwa na Daudi (18, 19)
Sheria ya Daudi kuhusu nyara (23, 24)
- 31 Kifo cha Sauli na wanawe watatu (1-13)

1 Sasa kulikuwa na mwanamume fulani kutoka Ramathaim-sofimu*^a katika eneo lenye milima la Efraimu^b aliyeitwa Elkana,^c mwana wa Yerohamu, mwana wa Elihu, mwana wa Tohu, mwana wa Sufu, Mwefraimu. **2** Alikuwa na wake wawili, mmoja aliitwa Hana na mwingine aliitwa Penina. Penina ali-

1:1 * Au "kutoka Rama, Msufu."

SURA YA 1

- a 1Sa 1:19
1Sa 7:15, 17
b Yos 16:5
c 1Nya 6:22, 27

Safu ya 2

- a Kut 23:14
Kut 34:23
Kum 12:5, 6
Yos 18:1
Amu 21:19
Lu 2:41
b 1Sa 2:12, 22
1Sa 4:17
c Hes 3:10
Kum 33:10
Mal 2:7

kuwa na watoto, lakini Hana hakuwa na watoto. **3** Mwaka baada ya mwaka mwanamume huyo alitoka katika jiji lake na kupanda kwenda Shilo kumwabudu* na kumtolea dhambihi Yehova wa majeshi.^a Wana wawili wa Eli, Hofni na Finehasi,^b walitumikia huko wakiwa makuhani wa Yehova.^c

1:3 * Au "kumwinamia."

4 Siku moja Elkana alipotoa dhabihu, alimpa Penina mke wake na wanawe na mabinti zake wote sehemu za dhabihu hiyo,^a 5 lakini akampa Hana sehemu ya pekee, kwa sababu alimpenda sana Hana; lakini Yehova hakuwa amempa watoto.* 6 Isitoshe, mke mwenzake alimdhiki daima ili kumkasirisha kwa sababu Yehova hakuwa amempa watoto. 7 Hivyo ndivyo alivyofanya mwaka baada ya mwaka; kila mara Hana alipopanda kwenda katika nyumba ya Yehova,^b mke mwenzake alimdhiki sana hivi kwamba alilia na kushindwa kula. 8 Lakini Elkana mume wake alimuuliza: “Hana, kwa nini unalia, na kwa nini huli chakula, na kwa nini umehuzunika sana?”* Je, mimi si bora kwako kuliko wana kumi?”

9 Basi siku moja Hana alisimama baada ya wao kumaliza kula na kunywa huko Shilo. Wakati huo, kuhani Eli alikuwa ameketi kwenye kiti karibu na mwimo wa mlango wa hekalu^c la Yehova. 10 Hana alikuwa na uchungu mwingi sana,* akaanza kusali kwa Yehova^d na kulia sana. 11 Naye akaweka nadhiri hii: “Ee Yehova wa majeshi, ikiwa utayona mateso yangu mimi mtumishi wako na kunikumbuka na usiponisahau mimi mtumishi wako, nawe unipe mtoto wa kiume,^e nitamtoa awe wa Yehova sikuzote za maisha yake, na hakuna wembe utakaogusa kichwa chake.”^f

1:5 *Tnn., “alikuwa amefunga tumbo lake la uzazi.” 1:8 *Au “na kwa nini moyo wako unahisi vibaya?” 1:9 *Yaani, hema la ibada. 1:10 *Au “uchungu nafisini.”

SURA YA 1

a Law 7:15

b Kum 16:16
1Sa 2:18,19c Kut 25:8
1Sa 3:3
2Sa 7:2d Zb 55:22
Zb 65:2

e Mwa 30:22

f Hes 6:5

Safu ya 2

a Zb 42:6
Zb 62:8
Zb 142:2

b 1Sa 1:11

c 1Sa 1:1

d 1Sa 1:11
Zb 66:19
Met 15:29e Mwa 5:29
Mwa 41:51
Kut 2:21, 22
Mt 1:21

12 Alipokuwa akisali kwa muda mrefu mbele za Yehova, Eli alikuwa akiangalia kinywa chake. 13 Hana alikuwa akisali moyoni mwake, midomo yake tu ndiyo iliyokuwa ikitetemeka, lakini sauti yake haikusikika. Basi Eli akafikiri kuwa amelewa. 14 Eli akamwambia, “Utaendelea kuwa mlevi mpaka lini? Acha kunywa divai.” 15 Ndipo Hana akamwambia, “Si-vyo, bwana wangu! Mimi ni mwanamke mwenye mka-zo mkubwa sana;* sijanya divai wala kinywaji chochote chenye kileo, bali ninaimwaga nafsi[#] yangu mbele za Yehova.^a 16 Usidhani mtumishi wako ni mwanamke asiye-faa kitu, kwa maana muda huo wote nimekuwa nikiongea katika uchungu mwingi na mate-so yangu.” 17 Ndipo Eli akamwambia, “Nenda kwa amani, na Mungu wa Israeli akupe ulichoomba.”^b 18 Basi Hana akamwambia, “Mtumishi wako na apate kibali machoni pako.” Ndipo mwanamke huyo akaenda zake, akala chakula, na uso wake haukuwa na huzu-ni tena.

19 Wakaamka asubuhi na mapema na kuinama mbele za Yehova, kisha wakarudi nyumbani kwao kule Rama.^c Elkana akafanya ngono na Hana mke wake, na Yehova akamkumbuka.^d 20 Katika muda wa mwaka mmoja* Hana alipata mimba, akazaa mwana na kumwita^e mwana huyo Samweli,[#] kwa maana alisema,

1:15 *Au “mwanamke aliyefadhika sana rohani.” [#]Angalia Kamusi, uku. 2012. 1:19 *Au “akamwelekeza fikira.” 1:20 *Au labda, “Wakati unao-faa ulipofika.” [#]Maana yake “Jina la Mungu.”

“nilimwomba kutoka kwa Yehova.”

21 Baada ya muda Elkana akaenda pamoja na familia yake yote kumtolea Yehova dhabihu^a ya kila mwaka na pia dhabihu yake ya nadhiri. **22** Lakini Hana hakwenda^b kwa sababu alimwambia hivi mume wake: “Mara tu nitakapomwachisha mvulana huyu kunyonya, nitampeleka mbele za Yehova, naye atabaki huko kuanzia wakati huo na kuendelea.”^c **23** Ndipo Elkana mume wake akamwambia, “Fanya unaloona linafaa.* Kaa nyumbani mpaka utakapomwachisha kunyonya. Yehova na atimize jambo ulilosema.” Basi mwanamke huyo akakaa nyumbani, akaendelea kumnyonyesha mwana wake mpaka alipomwachisha kunyonya.

24 Mara tu alipomwachisha kunyonya, alimpeleka Shilo pamoja na ng’ombe dume wa miaka mitatu, efa* moja ya unga, na mtungi mkubwa wa divai,^d naye pamoja na mvulana huyo wakafika katika nyumba ya Yehova huko Shilo.^e **25** Kisha wakamchinja huyo ng’ombe dume na kumpeleka mvulana huyo kwa Eli. **26** Ndipo Hana akasema, “Niwie radhi, bwana wangu! Kwa hakika kama unavyoishi,* bwana wangu, mimi ndiye yule mwanamke aliyekuwa amesimama pamoja nawe mahali hapa ili kusali kwa Yehova.^f **27** Nilisali nipate mvulana huyu, naye Yehova akanipa nilichoomba.^g **28** Sasa nami

1:23 *Tnn., “lililo jema machoni pako.”
1:24 *Efa ilikuwa sawa na lita 22 au kilogramu 13 hivi. Angalia Nyongeza B14.
1:26 *Au “Kwa uhai wa nafsi yako.”

SURA YA 1

a 1Sa 1:3

b Kum 16:16

c 1Sa 1:11
1Sa 2:11
2Nya 31:16

d Hes 15:8-10

e Yos 18:1

f 1Sa 1:15

g 1Sa 1:11,17
Zb 66:19

Safu ya 2

SURA YA 2

a Zb 13:6
Lu 1:46b Kut 15:11
Kum 4:35
Zb 73:25
Zb 86:8
Zb 89:6

c Kum 32:4

d Ayu 36:4
Ayu 37:16
Ro 11:33

e Isa 40:29

f Lu 1:53

g 1Sa 1:11,20

pia, ninamkabidhi Yehova mvulana huyu. Siku zake zote, amekabidhiwa kwa Yehova.”

Naye* akainama chini mbele za Yehova.

2 Kisha Hana akasema hivi katika sala:

“Moyo wangu unashangilia katika Yehova;^a

Pembe yangu imekwezwa* na Yehova.

Kinywa changu kimefunguliwa wazi dhidi ya maadui wangu,

Kwa maana ninashangilia kwa sababu ya matendo yako ya wokovu.

2 Hakuna aliye mtakatifu kama Yehova,

Hakuna mwingine isipokuwa wewe,^b

Na hakuna mwamba kama Mungu wetu.^c

3 Msiendeleo kuzungumza kwa kiburi;

Neno lolote la majivuno lisitoke vinywani mwenu,

Kwa maana Yehova ni Mungu wa ujuzi,^d

Naye hupima matendo kwa njia ya haki.

4 Pinde za mashujaa huvunjavunjwa,

Lakini wale wanaojikwaa hutiwa nguvu.^e

5 Walioshiba lazima waajiriwe ili wapate mkate,

Lakini wape njaa hawana njaa tena.^f

Aliye tasa amezaa watoto saba,^g

Lakini mwanamke aliyekuwa na wana wengi amechwa mpweke.*

1:28 *Inaonekana ni Elkana. 2:1 *Au “Nguvu zangu zimekwezwa.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:5 *Tnn., “amedhoofika.”

- 6** Yehova huua, naye huhifadhi uhai;*
Hushusha Kaburini,[#] naye hufufua.^a
- 7** Yehova humfanya mtu awe maskini, naye hutajirisha;^b
Hushusha, naye hukweza.^c
- 8** Humwinua mtu wa hali ya chini kutoka mavumbini; Humwinua maskini kutoka katika rundo la majivu,^{*d}
Ili awafanye wakae pamoja na wakuu,
Na kuwapa kiti cha heshima.
Nguzo za dunia ni za Yehova,^e
Naye huweka nchi inayozaa juu yake.
- 9** Hulinda hatua za washikamanifu wake;^f
Lakini waovu watanyamazishwa gizani,^g
Kwa maana mwanadamu hashindi kwa nguvu.^h
- 10** Yehova atawavunjavunja wale wanaopigana naye;^{*i}
Atanguruma dhidi yao kutoka mbinguni.^j
Yehova atahukumumu mpaka miisho ya dunia,^k
Atampa nguvu mfalme wake,^l
Na kuikweza pembe ya[#] mtiwa-mafuta wake.^m
- 11** Basi Elkana akaenda nyumbani kwake Rama, lakini yule mvulana akawa mhudumu wa* Yehovaⁿ chini ya ungalizi wa kuhani Eli.

2:6 *Au "huhuisa." #Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:8 *Au labda, "jaa la takataka; jalalani." 2:10 *Au labda, "Wale wanaoshindana na Yehova wataogopeshwa." #Au "nguvu za." Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:11 *Au "alikuwa akimtumikia."

SURA YA 2

a Kum 32:39
Ayu 14:13
Zb 30:3
Zb 49:15
Zb 68:20
Ho 13:14
Yoh 11:24
IKo 15:55

b Kum 8:18
Kum 28:12
2Nya 1:11, 12
Ayu 42:12
Met 10:22

c Zb 75:7

d Zb 113:5, 7
Lu 1:52

e Zb 102:25

f Zb 91:11
Zb 97:10
Zb 121:3

g Zb 37:28

h Zb 33:16
Zek 4:6

i Kut 15:6

j 1Sa 7:10
2Sa 22:14
Zb 18:13

k Zb 96:13
Mdo 17:31

l Zb 2:6
Zb 110:1
Mt 28:18

m Lu 1:69
Mdo 4:27

n 1Sa 1:11
1Sa 3:1, 15

Safu ya 2

a 1Sa 2:22

b Law 7:34

c Law 3:3-5

d Law 3:16
Law 7:25, 31

e 1Sa 2:29

f 1Sa 2:11
1Sa 3:15

g 2Sa 6:14

12 Sasa wana wa Eli walikuwa watu waovu;^a hawakumheshimu Yehova. **13** Hivi ndivyo walivyofanya kuhusu vitu vilivyoletwa na watu ambavyo vilikuwa haki ya makuhani:^b Kila mara mtu yeyote alipokuwa akitoa dhabihu, mtumishi wa kuhani alikuja na uma wenye meno matatu mkononi mwake nyama ilipokuwa iki-chemka, **14** naye aliutia kwa nguvu ndani ya beseni, chungu cha kupikia chenye mikono miwili, sufuria kubwa, au chungu cha kupikia chenye mkono mmoja. Nyama yoyote iliyoinuliwa na uma huo, ilichukuliwa na kuhani. Hivyo ndivyo walivyokuwa wakiwatendea Waisraeli wote waliokuja Shilo. **15** Pia, hata kabla ya mtu anayetoa dhabihu kuyafanya mafuta yafuke moshi,^c mtumishi wa kuhani alikuwa akija na kumwambia, "Mpe kuhani nyama akachome. Hatachukua nyama iliyochemshwa kutoka kwako, atachukua nyama mbichitu." **16** Mtu huyo alipomwambia, "Acha kwanza wahakikishe kwamba mafuta yamefuka moshi,^d kisha ujichukulie chochote upendacho,"* alisema: "Hapana, nipe sasa hivi; la si-vyo, nitaichukua kwa nguvu!" **17** Kwa hiyo dhambi ya watumishi hao ikawa kubwa sana mbele za Yehova,^e kwa maana watu hao hawakuheshimu dhabihu ya Yehova.

18 Basi Samweli alikuwa akihudumu^f mbele za Yehova, akiwa amevaa* efodi ya kitani,^g ingawa alikuwa mvulana tu. **19** Pia, mama yake alikuwa akimshonea joho

2:16 *Au "ambacho nafsi yako inatamani." 2:18 *Tnn., "amefungwa."

dogo lisilo na mikono na kumletea mwaka baada ya mwaka alipokuja na mume wake kutoa dhabihu ya kila mwaka.^a **20** Eli akambariki Elkana na mke wake akisema, “Yehova na akupe mtoto kutoa kwa mke huyu ili achukue nafasi ya yule aliyekabidhiwa kwa Yehova.”^b Kisha wakarudi nyumbani. **21** Yehova akamkazia uangalifu Hana, ili aweze kupata mimba;^c basi akazaa wana watatu zaidi na mabinti wawili. Naye mvulana Samweli akaendelea kukua mbele za Yehova.^d

22 Sasa Eli alikuwa amezeeka sana, lakini alikuwa amesikia mambo yote ambayo wanawe walikuwa wakiwatendea^e Waisraeli wote na jinsi waliivyokuwa wakilala na wanawake waliotumikia kwenye mlango wa hema la mkutano.^f **23** Alikuwa akiwaambia hivi: “Kwa nini mnaendelea kufanya mambo ya aina hii? Kwa maana mambo ninayosikia kuwahusu kutoka kwa watu wote ni mabaya. **24** Msifanye hivyo wanangu, kwa sababu habari ninazosikia zikienea miongoni mwa watu wa Yehova si nzuri. **25** Mwanadamu akimtendea dhambi mwanadamu mwenzake, mtu fulani anaweza kumsihi Yehova kwa niaba yake;” lakini mwanadamu akimtendea dhambi Yehova,^g ni nani anayeweza kusali kwa ajili yake?” Lakini walikataa kumsikiliza baba yao, kwa sababu Yehova alikuwa ameazimia kuwaua.^h **26** Lakini mvulana Samweli aliendelea kukua na kupendwa na Yehova na pia wanadamu.ⁱ

2:25 * Au labda, “Mungu atakuwa mpatanishi wake.”

SURA YA 2

a Kut 23:14
1Sa 1:3, 21

b 1Sa 1:27, 28

c Mwa 21:1, 2
1Sa 1:19

d 1Sa 2:26
1Sa 3:19

e 1Sa 2:12-17

f Kut 38:8
Law 21:6

g Hes 15:31
1Sa 2:17
1Sa 3:13, 14

h Met 29:1
Met 30:17

i 1Sa 2:21

Safu ya 2

a Kut 4:14, 27

b Kut 28:1
Law 8:12
Hes 17:5, 8

c Hes 18:7

d Law 2:3
Law 6:16
Law 10:14
Hes 5:9
Hes 18:9

e Kut 25:8
Yos 18:1
1Sa 1:3

f 1Sa 2:14-16

g Kut 28:43

h Zb 18:20
Zb 91:14

i 1Sa 3:14
1Sa 4:11, 18
1Sa 22:18
1Fa 2:27

27 Mtu wa Mungu alimjia Eli na kumwambia, “Yehova anasema hivi: ‘Je, sikujitambulisha waziwazi kwa watu wa nyumba ya baba yako walipokuwa Misri wakiwa watu-mwa wa nyumba ya Farao?’^a

28 Naye alichaguliwa kutoa katika makabila yote ya Israeli^b ili anitumikia akiwa kuhani wangu na kupanda juu ya madhabahu yangu^c kutoa dhabihu, kufukiza uvumba,* na kuvaa efodi mbele zangu; nami niliwapa watu wa nyumba ya babu yako dhabihu zote zinazochomwa kwa moto zilizotolewa na Waisraeli.^{#d}

29 Kwa nini ninyi wanaume mnadharau* dhabihu yangu na toleo langu ambalo nimeamuru katika makao yangu?^e Kwa nini unaendelea kuwaheshimu wana wako kuliko mimi kwa kujinenepesha kwa sehemu bora za kila dhabihu inayotolewa na watu wangu Waisraeli?^f

30 “Ndiyo sababu Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: “Hakika nilisema kwamba nyumba yako na nyumba ya babu yako itatembea mbele zangu daima.”^g Lakini sasa Yehova anatangaza hivi: “Ni jambo nililoweza kamwe kuwazia, kwa sababu wale wanaoniheshimu nitawaheshimu,^h lakini wale wanaonidharau watadharauliwa.” **31** Tazama! Siku zinakuja nitakapokata nguvu zako na za nyumba ya baba yako, hivi kwamba hakuna mwanamume yeyote wa nyumba yako atakayeishi na kuzeeka.ⁱ **32** Nawe

2:28 * Au labda, “kufanya moshi wa dhabihu upae juu.” [#]Tnn., “wana wa Israeli.” 2:29 *Tnn., “mnapiga teke.” 2:31 *Tnn., “mkono wenu na wa.”

utamwona adui katika makao yangu miongoni mwa mambo yote mema wanayofanyiwa Waisraeli,^a na kamwe haku-takuwa tena na mzee katika nyumba yako. **33** Mwanamu-me wako ambaye nitamwacha aendelee kutumikia kwenye madhabahu yangu atayadhoo-fisha macho yako na kukuletea huzuni, lakini idadi ku-bwa ya watu wa nyumba yako itauawa kwa upanga.^b **34** Na mambo yatakayowapata wana wako wawili, Hofni na Finehasi, yatakuwa ishara kwako: Wote wawili watakuwa siku ileile.^c **35** Kisha nitajiinulia kuhani mwaminifu.^d Atatenda kulingana na mapenzi ya moyo wangu;* nami nitamjengea nyumba ya kudumu, naye atatembea mbele ya mtiwama-futa wangu daima. **36** Mtu yeyote atakayebaki katika nyumba yako atakuja na kumwinamia ili alipwe pesa na kupata mkate, naye atasema: "Tafadhali, niweke katika nafasi yoyote ya ukuhani ili nile kipande cha mkate."^e

3 Wakati huo, mvulana Samweli alikuwa akimhudumia^f Yehova chini ya uangalizi wa Eli, lakini neno la Yehova lilikuwa haba siku hizo; maono^g hayakuwa mengi.

2 Siku moja Eli alikuwa amelala mahali alipozoea kulala, na macho yake yalikuwa yamedhoofika; hange-weza kuona.^h **3** Taa ya Munguⁱ haikuwa imezimwa, na Samweli alikuwa amelala katika hekalu^{*j} la Yehova, mahali ambapo Sanduku la Mungu lilikuwa. **4** Kisha Yehova aka-

2:35 *Au "kilicho katika moyo wangu na nafsi yangu." 3:3 *Yaani, hema la ibada.

SURA YA 2

a Zb 78:60, 61

b 1Sa 22:18, 21

c 1Sa 4:11, 17

d 1Fa 2:27, 35
1Nya 29:22e Law 2:3
Hes 5:9

SURA YA 3

f 1Sa 2:11, 18

g Hes 12:6
1Nya 17:15

h 1Sa 4:15

i Law 24:2

j 1Sa 1:9
1Sa 3:15

Safu ya 2

a Amo 3:7

b 1Sa 4:17

c Hes 23:19
1Sa 2:31-34
Isa 55:10, 11

mwita Samweli. Samweli akajibu: "Mimi hapa." **5** Akaki-ambia kwa Eli na kusema, "Nimekuja, kwa kuwa umeniita." Lakini Eli akasema: "Sikukuita. Rudi ukalale." Basi akaenda kulala. **6** Yehova akaita tena: "Samweli!" Basi Samweli akaamka na kwenda kwa Eli, akamwambia: "Nimekuja, kwa kuwa umeniita." Lakini Eli akamwambia: "Sikukuita, mwanangu. Rudi ukalale." **7** (Wakati huo Samweli alikuwa bado hajamjua Yehova, na neno la Yehova lilikuwa bado halijafunuliwa kwa ke.)^a **8** Yehova akaita tena mara ya tatu: "Samweli!" Basi akaamka, akaenda kwa Eli na kumwambia: "Nimekuja, kwa kuwa umeniita."

Ndipo Eli akatambua kwamba ni Yehova aliyekuwa akimwita mvulana huyo. **9** Kwa hiyo Eli akamwambia Samweli: "Rudi ukalale, na akikuita, mwambie, 'Sema, Yehova, kwa maana mtumishi wako anasikiliza.'" Basi Samweli akaenda na kulala mahali alipokuwa akilala.

10 Yehova akaja na kusima mahali hapo, akaita kama alivyofanya awali: "Samweli, Samweli!" Ndipo Samweli akajibu: "Sema, kwa maana mtumishi wako anasikiliza." **11** Yehova akamwambia Samweli: "Tazama! Ninafanya jambo fulani katika Israeli ambalo litawasha masikio yote mawili ya mtu yeyote atakayelisikia.^b **12** Siku hiyo nitamtendea Eli mambo yote niliyosema kuhusu nyumba yake, kuanzia mwanzo mpaka mwisho.^c **13** Ni lazima umwambie kwamba ninaitolea nyumba yake hukumu ya

kudumu kwa sababu ya dhambi ambayo anaijua,^a kwa maana wanawe wanamtukana Mungu,^b lakini hajawakemea.^c **14** Ndiyo sababu nimejiapia nyumba ya Eli kwamba dhambi ya nyumba ya Eli haitafunikwa kamwe kwa dhahibu au kwa matoleo.”^d

15 Samweli akaendelea kulala mpaka asubuhi; kisha akafungua milango ya nyumba ya Yehova. Samweli akaogopa kumwambia Eli maono hayo. **16** Lakini Eli akaagiza Samweli aitwe, akamwambia: “Samweli, mwanangu!” Naye akasema: “Naam.” **17** Eli akamuuliza, “Alikupa ujumbe gani? Tafadhali, usinifiche. Mungu na akuadhibu, tena vikali, ukinificha neno hata moja kati ya maneno yote ambayo alikwambia.” **18** Basi Samweli akamwambia kila jambo, wala hakumficha lolote. Eli akasema: “Ni Yehova. Na afanye yaliyo mema machoni pake.”

19 Samweli akaendelea kuka, na Yehova mwenyewe alikuwa pamoja naye^e na hakuruhusu neno lolote kati ya maneno yake yote likose kutimia.* **20** Waisraeli wote kuanzia Dani mpaka Beer-sheba wakapata habari kwamba Samweli alikuwa amewekwa rasmi kuwa nabii wa Yehova. **21** Na Yehova akaendelea kutokea huko Shilo, kwa kuwa Yehova alijidhihirisha kwa Samweli huko Shilo kwa neno lake Yehova.^f

4 Na neno la Samweli likawafikia Waisraeli wote.

Kisha Waisraeli wakaenda kupigana na Wafilisti; wakapi-

3:19 *Tnn., “lianguke ardhini.”

SURA YA 3

a 1Sa 2:22, 23
Yoh 15:22
Yak 4:17

b Hes 15:30
1Sa 2:12, 17

c Mhu 8:11

d 1Sa 4:11
1Sa 22:21
1Fa 2:27

e 1Sa 2:21

f 1Sa 3:1, 4
Zb 99:6

Safu ya 2

SURA YA 4

a Kum 28:15, 25
Kum 32:30
Amu 2:14

b 2Sa 15:25

c Kut 25:18
Hes 7:89
Zfa 19:15
Zb 80:1

d 1Sa 2:12

e Kut 14:25
Kut 15:14

ga kambi kando ya Ebenezeri, na Wafilisti walikuwa wamepiga kambi Afeki. **2** Wafilisti wakajipanga kivita ili kupigana na Waisraeli, lakini mambo yakawaendea vibaya Waisraeli vitani, nao wakashindwa na Wafilisti, ambao waliwaua wanaume wapatao 4,000 kwenye uwanja wa vita. **3** Watu waliporudi kambini, wazee wa Israeli wakasema hivi: “Kwa nini Yehova ameruhusu tushindwe leo na Wafilisti?}*^a Na tujichukulie sanduku la agano la Yehova kutoka Shilo,^b twendene nalo ili lituokoe kutoka mikononi mwa maadui wetu.”

4 Basi watu wakawatuma wanaume kwenda Shilo, nao wakachukua kutoka huko sanduku la agano la Yehova wa majeshi, anayeketi akiwa mfalme juu ya* makerubi.^c Na wana wawili wa Eli, yaani, Hofni na Finehasi,^d walikuwa huko pia pamoja na sanduku la agano la Mungu wa kweli.

5 Mara tu sanduku la agano la Yehova lilipofika kambini, Waisraeli wote wakaanza kupiga kelele kwa sauti kubwa, hivi kwamba dunia ikatikisika. **6** Wafilisti waliposikia kelele hizo, wakasema: “Kwa nini kuna kelele nyingi sana katika kambi ya Waebrania?” Hatimaye wakapata habari kwamba Sanduku la Yehova lilikuwa limeletwa kambini. **7** Wafilisti wakaogopa, kwa sababu walisema: “Mungu amekuja kambini!”^e Basi wakasema: “Ole wetu, kwa maana jambo kama hili halijawahi kamwe kutokea! **8** Ole wetu! Ni nani atakayetuokoa kutoka katika

4:3 *Tnn., “Kwa nini Yehova ametushinda leo kwa kuwatumia Wafilisti?” 4:4 *Au labda, “katikati ya.”

mkono wa Mungu huyu mkuu? Huyu ndiye Mungu aliyewachinja Wamisri kwa kila aina ya mapigo nyikani.^a **9** Iweni jasisiri na kutenda kama wanaume, enyi Wafilisti, ili msiwatumikie Waebrania kama waliyovowatumikia ninyi.^b Tendeni kama wanaume, mkapigane!” **10** Basi Wafilisti wakapigana nao, na Waisraeli wakashindwa,^c na kila mmoja wao akakimbilia katika hema lake. Yalikuwa mauaji makubwa sana; wanajeshi 30,000 wa Israeli wanaotembea kwa miguu waliuawa. **11** Isitoshe, Sanduku la Mungu lilitekwwa, na wana wawili wa Eli, Hofni na Finehasi, wakafa.^d

12 Mtu fulani Mbenjamini akakimbia kutoka katika uwanja wa vita, akafika Shilo siku hiyo akiwa amevaa nguo zilizoraruka na akiwa na mavumbi kichwani.^e **13** Mtu huyo alipofika, Eli alikuwa ameketi kwenye kiti kando ya barabara akitazama barabarani, kwa kuwa moyo wake ulikuwa ukitetemeka kwa sababu ya Sanduku la Mungu wa kweli.^f Mtu huyo akaingia jijini kutangaza habari hizo, na jiji lote likaanza kulia kwa sauti kubwa. **14** Eli aliposikia vilio hivyo, akauliza: “Kelele hizo za machafuko ni za nini?” Mtu huyohuyo akafika haraka na kumwambia Eli habari hizo. **15** (Wakati huo Eli alikuwa na umri wa miaka 98, naye alikodoa macho yake mbele, lakini hakuweza kuona.)^g **16** Kisha mtu huyo akamwambia Eli: “Ni mimi niliyetoka katika uwanja wa vita! Nimekimbia kutoka katika uwanja wa vita leo hii.” Basi amauliza: “Mwanangu, ilikuwaje?”

SURA YA 4

a Kut 7:5
Zb 78:43, 51

b Kum 28:48
Amu 10:7
Amu 13:1

c Law 26:14, 17
Kum 28:25
1Sa 4:2

d 1Sa 2:31, 34
1Sa 4:3, 17
Zb 78:61, 64

e Yos 7:6

f 1Sa 4:4

g 1Sa 3:2

Safu ya 2

a 1Sa 3:11

b 1Sa 2:34

c 1Sa 4:10, 11

d 1Sa 14:3

e Zb 78:61

f 1Sa 2:32, 34
1Sa 4:5, 11

g 1Sa 4:11
Yer 7:12

17 Basi mtu huyo aliyeleta habari akasimulia hivi: “Waisraeli wamewakimbia Wafilisti, na watu wameshindwa vibaya sana;^a pia, wana wako wawili, Hofni na Finehasi, wamekufa,^b na Sanduku la Mungu wa kweli limetekwa.”^c

18 Mara tu alipotaja Sanduku la Mungu wa kweli, Eli akaanguka nyuma kutoka kwenye kiti chake kando ya lango, na shingo yake ikavunjika naye akafa, kwa sababu alikuwa amezeeka na alikuwa mzito. Alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka 40. **19** Binti mkwe wake, yaani, mke wa Finehasi, alikuwa mjamzito naye alikuwa karibu kuzaa. Aliposikia kwamba Sanduku la Mungu wa kweli limetekwa na kwamba baba mkwe wake na mume wake wamekufa, akainama na kwa ghafla akapata uchungu wa kuzaa, kisha akazaa. **20** Alipokuwa akifa, wanawake waliokuwa wamesimama kando yake wakasema: “Usiogope, kwa maana umezaa mwana.” Hakujibu wala kukazia fikira jambo hilo.* **21** Lakinini alimwita mvulana huyo Ikabodi,^{*d} akisema: “Utukufu umeondoka Israeli na kwenda uhamishoni,”^e alisema hivyo kwa sababu Sanduku la Mungu wa kweli lilitekwwa na kwa sababu ya mambo yaliyompata baba mkwe wake na mume wake.^f **22** Basi akasema: “Utukufu umeondoka Israeli na kwenda uhamishoni, kwa sababu Sanduku la Mungu wa kweli limetekwa.”^g

4:20 *Au “wala kutia moyoni jambo hilo.” 4:21 *Maana yake “Utukufu uko Wapi?”

5 Wafilisti walipoliteka Sanduku la Mungu^a wa kweli walilibeba kutoka Ebenezeri mpaka Ashdodi. **2** Wafilisti wakalichukua Sanduku la Mungu wa kweli, wakaliingiza ndani ya nyumba ya* Dagoni na kuliweka kando ya Dagoni.^b **3** Siku iliyofuata Waashdodi walipoamka asubuhi na mapema, walimkuta Dagoni ameanguka kifudufudi mbele ya Sanduku la Yehova.^c Basi wakamchukua Dagoni na kumrudisha mahali pake.^d **4** Walipoamka asubuhi na mapema siku iliyofuata, walimkuta Dagoni ameanguka kifudufudi mbele ya Sanduku la Yehova. Kichwa cha Dagoni na vitanga vya mikono yake miwili vilikuwa vimekatwa, navyo vilikuwa chini kwenye kizingiti. Ni sehemu tu yenye umbo la samaki ndiyo iliyo-baki.* **5** Ndiyo sababu mpaka leo hii, makuhani wa Dagoni na wote wanaoingia katika nyumba ya Dagoni hawakanyagi kizingiti cha Dagoni kule Ashdodi.

6 Mkono wa Yehova uliwaadhibu vikali* Waashdodi, naye akawaangamiza kwa kuleta bawasiri[#] huko Ashdodi na katika maeneo yake.^e **7** Watu wa Ashdodi walipona mambo yaliyokuwa yakitukia wakasema: "Msiruhusu Sanduku la Mungu wa Israeli likae pamoja nasi, kwa sababu mkono wake umetuadhibu vikali sisi pamoja na mungu wetu Dagoni." **8** Basi wakatuma ujumbe na kuwakusanya watawala wote wa Wafilisti

5:2 *Au "hekalu la." 5:4 *Tnn., "Ni Dagoni tu aliyebaki." 5:6 *Tnn., "ulikuwa mzito dhidi ya." ^aAu "ugonjwa wa puru."

SURA YA 5

a 1Sa 4:11

b Amu 16:23
1Nya 10:8-10c Kut 12:12
1Nya 16:26
Zb 97:7

d Isa 46:6,7

e 1Sa 6:5,6

Safu ya 2

a 1Sa 17:4

b 1Sa 5:6

c Yos 15:20,45
2Fa 1:2
Amo 1:8

d 1Sa 5:7

e 1Sa 5:6,9

SURA YA 6

f 1Sa 4:11
1Sa 5:1
Zb 78:61g Kum 18:9,10
Isa 2:6

na kuwauliza: "Tulifanyie nini Sanduku la Mungu wa Israeli?" Wakajibu: "Acheni Sanduku la Mungu wa Israeli lihamishiwe kule Gathi."^a Basi wakalihamishia huko Sanduku la Mungu wa Israeli.

9 Baada ya kulihamishia huko, mkono wa Yehova uka-ja dhidi ya jiji hilo, na kusababisha hofu kubwa. Akawapiga wanaume wa jiji hilo, kuanzia mdogo mpaka mkubwa, wakatokwa na majipu ya bawasiri.^b **10** Basi wakalipeleka Sanduku la Mungu wa kweli kule Ekroni,^c lakini mara tu Sanduku la Mungu wa kweli lilipofika Ekroni, Waekroni wakaanza kulia kwa sauti wakisema: "Wametuletea Sanduku la Mungu wa Israeli ili watue sisi pamoja na watu wetu!"^d **11** Kwa hiyo wakatuma ujumbe na kuwakusanya watawala wote wa Wafilisti na kuwaambia: "Liondoeni hapa Sanduku la Mungu wa Israeli; lirudisheni mahali pake ili sisi pamoja na watu wetu tusiuawe." Kwa maana hofu ya kifo ilikuwa imeenea katika jiji lote; mkono wa Mungu wa kweli ulikuwa umewaadhibu vikali sana watu wa jiji hilo,^e **12** na watu ambao hawakufa walikuwa wamepigwa na bawasiri. Na kilio cha jiji hilo cha kuomba msaada kikapanda mpaka mbinguni.

6 Sanduku^f la Yehova likaa katika eneo la Wafilisti kwa miezi saba. **2** Wafilisti wakawaita makuhani na wabashiri,^g wakawauliza: "Tulifanyie nini Sanduku la Yehova? Tuambieni jinsi tunavyopaswa kulirudisha mahali pake." **3** Wakajibu: "Mkilirudisha sanduku la agano la Ye-

hova, Mungu wa Israeli, msilirudishe bila dhabihu. Kwa vyovyote vile mnapaswa kumrudishia pamoja na dhabihu ya hatia.^a Ndipo tu mtakapoponywa, nanyi mtajulishwa kwa nini mkono wake unaendelea kuwaadhibu.” **4** Basi wakauliza: “Tunapaswa kumpelekea dhabihu gani ya hatia?” Wakasema: “Kulingana na idadi ya watawala wa Wafilisti,^b pelekeni bawasiri tano za dhahabu na panya watawala wa dhahabu, kwa maana kila mmoja wenu pamoja na watawala wenu wamepatwa na pigo lilelile. **5** Mnapaswa kutengeneza sanamu za bawasiri zenu na sanamu za panya^c wenu wanaoiharibu nchi, nanyi mnapaswa kumheshimu Mungu wa Israeli. Labda atapunguza adhabu ya mkono wake dhidi yenu na dhidi ya mungu wenu na nchi yenu.^d **6** Kwa nini mfanye mioyo yenu iwe migumu kama Wamisri na Farao walivyofanya mioyo yao kuwa migumu?^e Alipowaadhibu vikali,^f walilazimika kuwaruhusu Waisraeli waende zao, nao wakaondoka.^g **7** Sasa tayarisheni gari jipya la kukotwa na ng’ombe wawili wanaonyonyesha ambao hawajawahi kamwe kufungwa nira. Kisha muwafunge ng’ombe hao kwenye gari hilo, lakini muwarudishe ndama wao nyumbani ili wasiwafuate. **8** Chukueni Sanduku la Yehova na kuliweka juu ya gari hilo, nanyi wekeni ndani ya sanduku lingine kando yake vitu vya dhahabu mnavyompelekea kuwa dhabihu ya hatia.^h Kisha mliache gari liende **9** huku mkilita-

SURA YA 6

a 1Sa 6:4,17

b Yos 13:2,3
1Sa 6:16

c 1Sa 6:18

d 1Sa 5:6,11

e Kut 7:13
Kut 8:15
Kut 14:17f Kut 9:14,16
Ro 9:17,18g Kut 6:1
Kut 11:1
Kut 12:33

h 1Sa 6:3,4

Safu ya 2

a Yos 15:10,12
Yos 21:8,16
2Nya 28:18

b 1Sa 6:8,9

c 1Sa 6:7

d Hes 3:30,31

zama: Ikiwa litapanda kwenye barabara inayoelekea Beth-shemeshi,^a kwenye eneo lake, basi yeye ndiye ametutendea uovu huu mkubwa. Lakini lisipopanda huko, tutajua kwamba si mkono wake uliotuadhibu; ni msiba wa kawaida tu uliotupata.”

10 Watu hao wakafanya hivyo. Wakachukua ng’ombe wawili wanaonyonyesha, wakawafunga kwenye gari hilo, na kuwafungia ndama wa nyumbani ndani ya zizi.

11 Kisha wakaliweka Sanduku la Yehova juu ya gari hilo, pamoja na sanduku lenye panya wa dhahabu na sanamu za bawasiri zao. **12** Ng’ombe hao wakaenda moja kwa moja kwenye barabara inayoelekea Beth-shemeshi.^b Walibaki kwenye barabara hiyo kuu, nao walikuwa wakilia walipo kuwa wakienda; hawakugeuka kulia wala kushoto. Wakati huo wote, watawala wa Wafilisti walikuwa wakitembea nyuma yao hadi kwenye mpaka wa Beth-shemeshi. **13** Watu wa Beth-shemeshi walikuwa wakivuna ngano katika bonde tambarare. Walipoinua macho yao na kuona lile Sanduku, wakashangilia sana kuliona. **14** Gari hilo likafika kwenye shamba la Yoshua Mbeth-shemeshi, likasimama karibu na jiwe kubwa. Basi wakapasua mbaao za gari hilo, na kuwatoa ng’ombe^c hao kuwa dhabihu ya kuteketezwa kwa Yehova.

15 Walawi^d wakalishusha Sanduku la Yehova na sanduku lililokuwa kando yake ambalo lilikuwa na vile vitu vya dhahabu, wakaviweka juu

ya lile jiwe kubwa. Watu wa Beth-shemeshi^a wakamtolea Yehova dhabihu za kutekelezwa na dhabihu nyingine siku hiyo.

16 Watawala watano wa Wafilisti walipoona hayo, wakarudi Ekroni siku hiyo.

17 Basi hizi ndizo bawasiri za dhahabu ambazo Wafilisti walimletea Yehova kuwa dhabihu ya hatia:^b moja kwa ajili ya Ashdodi,^c moja kwa ajili ya Gaza, moja kwa ajili ya Ashkeloni, moja kwa ajili ya Gathi,^d moja kwa ajili ya Ekroni.^e **18** Na idadi ya panya wa dhahabu ililingana na idadi ya majiji yote ya Wafilisti ya wale watawala watano, majiji yenye ngome na vijiji vya mashambani visivyo na kuta.

Na jiwe kubwa ambalo waliweka Sanduku la Yehova juu yake ni ushahidi mpaka leo katika shamba la Yohua Mbeth-shemeshi. **19** Lakini Mungu akawaua watu wa Beth-shemeshi, kwa sababu walilitazama Sanduku la Yehova. Aliwaua watu 50,070* miongoni mwao, basi watu wakaanza kuomboleza kwa sababu Yehova alikuwa amewaua kwa mauaji makubwa.^f **20** Kwa hiyo watu wa Beth-shemeshi wakauliza: "Ninani atakayeweza kusimama mbele za Yehova, huyi Mungu mtakatifu,^g naye atienda kwa nani akitoka kwe-tu?"^h **21** Basi wakawatuma wajumbe kwa wakaaji wa Kiriath-yearimu,ⁱ wakisema: "Wafilisti wamelirudisha Sanduku la Yehova. Shukeni mlichukue na kupanda nalo."^j

6:19 *Tnn., "wanaume 70, wanaume 50,000."

SURA YA 6

a Yos 21:8,16

b 1Sa 6:4

c 1Sa 5:1

d 1Sa 5:8

e Amu 1:18
1Sa 5:10f Hes 4:15,20
1Nya 13:10

g Law 11:45

h Hes 17:12,13
2Sa 6:8,9
Zb 76:7i Yos 18:14
1Nya 13:5,6j 1Nya 16:1
2Nya 1:4

Safu ya 2

SURA YA 7

a 2Sa 6:2,4
1Nya 13:5,7

b Ne 9:28

c 1Sa 12:24

d Yos 24:14,23
Amu 3:7e Amu 2:13
Amu 10:6
1Fa 11:33f Kum 10:20
Kum 13:4
Lu 4:8

g Kum 28:1

h Amu 10:16

i Amu 20:1
1Sa 10:17
2Fa 25:23
Yer 40:6j 1Sa 12:23
Yak 5:16k 2Nya 20:3
Ne 9:1
Yoe 2:12

l Amu 10:10

m Amu 2:18

n Yos 13:2,3
1Sa 6:4

7 Basi watu wa Kiriath-yearimu wakaja na kuli-chukua Sanduku la Yehova na kulipandisha katika nyumba ya Abinadabu^a juu ya kilima, nao wakamtakasa Eleazari mwanawe ili alilinde Sanduku la Yehova.

2 Muda mrefu ulipita, jumla ya miaka 20, tangu Sanduku hilo lilipoletwa Kiriath-yearimu, na nyumba yote ya Israeli kuanza kumtafuta* Yehova.^b **3** Kisha Samweli akaiambia nyumba yote ya Israeli: "Ikiwa mnamrudia Yehova kwa moyo wenu wote,^c ondoeni miungu ya kigeni^d na sanamu za Ashtorethi^e kuto-ka kati yenu, nanyi elekezeni moyo wenu kwa Yehova bila kuyumbayumba na kumtumikia yeye peke yake,^f naye atawaoka kutoka mikononi mwa Wafilisti."^g **4** Kwa hiyo Waisraeli wakaondoa Mabaali na sanamu za Ashtorethi na kumtumikia Yehova peke yake.^h

5 Kisha Samweli akasema: "Wakusanyeni Waisraeli wote Mispā,ⁱ nami nitasali kwa Yehova kwa ajili yenu."^j **6** Basi wakakusanyika pamoja huko Mispā, nao wakachota maji na kuyamwaga mbele za Yehova na kufunga siku hiyo.^k Wakiwa huko wakasema: "Tumemte-ndea dhambi Yehova."^l Naye Samweli akaanza kutumikia akiwa mwamuzi^m wa Waisraeli huko Mispā.

7 Wafilisti waliposikia kwamba Waisraeli wamekusanyika pamoja Mispā, watawala wa Wafilistiⁿ wakapanda kwen-nda kuwashambulia Waisraeli. Waisraeli waliposikia habari hizo, waliogopa kwa saba-

7:2 *Au "kuomboleza mbele za."

bu ya Wafilisti. **8** Kwa hiyo Waisraeli wakamwambia Samweli: “Usiache kumwomba Yehova Mungu wetu atusaidie^a na kutuokoa kutoka mikononi mwa Wafilisti.” **9** Ndiipo Samweli akachukua mwana-kondoo anayenyonya, akamtoa kwa Yehova kuwa dhahihu nzima ya kuteketezwa;^b na Samweli akamwomba Yehova awasaidie Waisraeli, naye Yehova akamjibu.^c **10** Samweli alipokuwa akitoa dhahihu hiyo ya kuteketezwa, Wafilisti wakakaribia ili kupigana na Waisraeli. Basi siku hiyo Yehova akawaletea Wafilisti mngurumo mkubwa sana,^d Naye akawavuruga,^e wakashindwa mbele ya Waisraeli.^f **11** Ndiipo wanaume wa Israeli wakatoka Misp na kuwafuatia Wafilisti, wakawaua mpaka upande wa kusini wa Beth-kari. **12** Kisha Samweli akachukua jiwe^g na kuliweka kati ya Misp na Yeshana, akaliita Ebenezeri,^{*} kwa kuwa alisema: “Yehova ametusaidia mpaka sasa.”^h **13** Kwa hiyo Wafilisti wakashindwa, nao hawakuja tena katika eneo la Waisraeli;ⁱ na mkono wa Yehova ukaendelea kuwashinda Wafilisti siku zote za Samweli.^j **14** Pia, majiji ambayo Wafilisti walikuwa wamechukua kutoka kwa Waisraeli yalirudishwa kwa Waisraeli, kuanzia Ekroni mpaka Gathi, na Waisraeli wakayakomboa maeneo yao kutoka mikononi mwa Wafilisti.

Pia kukawa na amani kati ya Waisraeli na Waamori.^k

15 Samweli akaendelea kuwa mwamuzi wa Israeli mai-

SURA YA 7

a 1Sa 12:19

Isa 37:4

b Law 1:10

c Zb 99:6

d 1Sa 2:10

2Sa 22:14

e Yos 10:10

Amu 4:15

f Kum 20:4

Kum 28:7

g Yos 4:9

Yos 24:26

h Zb 44:3

i 1Sa 9:16

1Sa 13:5

j 1Sa 14:22, 23

1Sa 17:51

k Mwa 15:18, 21

Safu ya 2

a 1Sa 3:20

1Sa 12:11

1Sa 25:1

Mdo 13:20

b Yos 16:1

c Yos 15:7, 12

1Sa 11:15

d 1Sa 7:5

e 1Sa 1:1

1Sa 8:4

1Sa 19:18

f Kut 20:25

SURA YA 8

g 1Nya 6:28

h Kut 18:21

i Kut 23:8

Kum 16:19

Zb 15:5

Met 29:4

j Kum 24:17

k Kum 17:14, 15

1Sa 12:13

Mdo 13:21

l Amu 8:23

1Sa 10:19

1Sa 12:12

Isa 33:22

m Kum 9:24

n Amu 2:19

sha yake yote.^a **16** Kila mwaka alisafiri na kuzunguka Betheli,^b Gilgali,^c na Misp,^d naye alikuwa mwamuzi wa Israeli katika maeneo hayo yote. **17** Lakini alikuwa akirudi Rama,^e kwa sababu nyumba yake ilikuwa huko, na huko pia alitumikia akiwa mwamuzi wa Israeli. Alimjengea Yehova madhabahu huko.^f

8 Samweli alipokuwa amezeeka, aliwaweka wanaume kuwa waamuzi wa Israeli. **2** Mwana wake wa kwanza aliitwa Yoeli, na wa pili aliitwa Abiya;^g walikuwa waamuzi huko Beer-sheba. **3** Lakini wanawe hawakufuata njia zake; walikuwa na mwelekeo wa kujitafutia faida isiyo ya haki,^h walipokea rushwa,ⁱ na kupotosha haki.^j

4 Baada ya muda wazee wote wa Waisraeli walikusanyika pamoja na kuja kumwona Samweli huko Rama. **5** Wakamwambia: “Tazama! Mezeeka, lakini wana wako hawatembeji katika njia zako. Basi tuchagulie mfalme awe mwamuzi wetu kama mataifa mengine yote.”^k **6** Lakini Samweli hakufurahi waliposema: “Tupe mfalme awe mwamuzi wetu.” Kwa hiyo Samweli akasali kwa Yehova, **7** Yehova akamwambia Samweli: “Sikiliza mambo yote ambayo watu wanakuambia; kwa maana hawajakukataa wewe, bali wamenikataa mimi nsiwe mfalme wao.^l **8** Wanatenda kama walivyozea kute nda tangu nilipowatoa Misri mpaka leo hii; wamekuwa wakiniacha^m na kuabudu miungu mingine,ⁿ na hivyo ndivyo wanavyokutendea wewe

pia. **9** Sasa wasikilize. Hata hivyo, unapaswa kuwaonya vikali; waambie mambo ambayo mfalme atakayewatawala atakuwa na haki ya kudai.”

10 Basi Samweli akawaambia maneno yote ya Yehova watu waliokuwa wakimwomba awape mfalme. **11** Aka-sema: “Mfalme atakayewatawala atakuwa na haki ya kudai mambo haya:^a Atawachukua wana wenu^b na kuwafanya wawe waendeshaji wa magari yake ya farasi^c na wapanda farasi wake,^d na baadhi yao watalazimika kukimbia mbele ya magari yake. **12** Naye atajichagulia wakuu wa maelfu^e na wakuu wa hamsini,^f na baadhi yao watamlimia mashamba yake,^g watavuna mazao yake,^h na kutengeneza silaha zake za vita na vifaa vya magari yake.ⁱ **13** Atachukua mabinti wenu na kuwafanya kuwa watengenezaji wa marashi,* wapishi, na waokaji.^j **14** Atachukua mashamba yenu bora, mashamba yenu bora ya mizabibu, na mashamba yenu bora ya mizeituni^k na kuwapa watumishi wake. **15** Atachukua sehemu ya kumi ya mashamba yenu ya nafaka na mashamba yenu ya mizabibu na kuwapa maofisa wa makao yake na watumishi wake. **16** Naye atachukua watumishi wenu wa kiume na wa kike, ng’ombe wenu walio bora, na punda wenu na kuwatumia kufanya kazi zake.^l **17** Atachukua sehemu ya kumi ya kondoo wenu na mbuzi wenu,^m nanyi mtakuwa watumishi wake. **18** Siku itafika mtaka-

8:13 *Au “wachanganyaji wa manukato.”

SURA YA 8

a 1Sa 10:25

b 1Sa 14:52

c 1Fa 9:22
1Fa 10:26

d 1Fa 4:26

e 2Sa 18:1
1Nya 27:1

f 2Fa 1:14

g 1Nya 27:26

h 1Fa 4:7

i 1Fa 4:26

j 1Fa 4:22

k 1Nya 27:28, 31

l 1Fa 5:15, 16

m 1Fa 4:22, 23

Safu ya 2

a 1Fa 12:3, 4

b 1Sa 8:7
Ho 13:11

SURA YA 9

c 1Sa 14:51
1Nya 8:33
Mto 13:21

d Amu 21:17

e 1Sa 11:15
1Sa 13:13
1Sa 15:26
1Sa 28:7
1Sa 31:4
2Sa 1:23

polia kwa sababu ya mfalme ambaye mljichagulia wenyewe,^a lakini Yehova hatawajibu siku hiyo.”

19 Hata hivyo, watu waka-kataa kusikiliza mambo ambayo Samweli aliwaambia, wakasema: “Hatutaki, tumeazimia kuwa na mfalme wa kututawala. **20** Kisha tutakuwa kama mataifa mengine yote, na mfalme wetu atakuwa mwamuzi wetu, atatuongoza, na kupigana vita vyetu.” **21** Baada ya Samweli kusi-kia maneno yote ya watu, akayarudia masikioni mwa Yehova. **22** Yehova akamwambia Samweli: “Wasikilize, na uweke mfalme wa kuwatawala.”^b Basi Samweli akawaambia Waisraeli: “Kila mmoja wenu arudi katika jiji lake.”

9 Kulikuwa na mtu wa Benjamini aliyelitwa Kishi,^c mwana wa Abieli, mwana wa Zerori mwana wa Bekorathi mwana wa Afia, Mbenjamini^d aliyekuwa tajiri sana. **2** Alikuwa na mwana aliyelitwa Sauli,^e kijana mwenye sura nzuri, hakuna mwanamume yeyote kati ya Waisraeli aliyekuwa na sura nzuri kuliko yeye, na aliposimama watu wote walimfikia mabegani.

3 Punda wa Kishi baba ya Sauli walipopotea, Kishi alimwambia hivi Sauli mwana-we: “Tafadhali mchukue mtumishi mmoja mwende mka-watafute punda.” **4** Wakapita katika eneo lenye milima la Efraimu na katika nchi ya Shalisha, lakini hawakuwapata. Wakasafiri kupitia nchi ya Shaalimu, lakini hawakuwapata punda huko. Wakapita katika nchi yote ya Wabenjamini, lakini hawakuwapata.

5 Wakafika katika nchi ya Sufu, Sauli akamwambia mtumishi wake aliyekuwa pamoja naye: “Njoo, acha turudi, ili baba yangu asianze kutuhangaika badala ya kuhangaika punda.”^a 6 Lakini mtumishi huyo akamwambia: “Tazama! Kuna mtu wa Mungu katika jiji hili, mtu anayeheshimiwa. Kila jambo analosema lazima litimie.”^b Twende huko sasa. Labda anaweza kutuambia njia ya kufuata.” 7 Basi Sauli akamwambia hivi mtumishi wake: “Tukienda, tutampelekea nini mtu huyo? Mifuko yetu haina mikate; hatuna zawadi yoyote ya kumpelekea huyo mtu wa Mungu wa kweli. Tuna nini?” 8 Basi mtumishi huyo akamjibu hivi Sauli: “Tazama! Nimebeba mikononi mwangu robo ya shekeli* ya fedha. Nitampa huyo mtu wa Mungu wa kweli, naye atatuambia njia ya kufuata.” 9 (Zamani katika Israeli, mtu alikuwa akisema hivi alipoenda kutafuta mwongozo wa Mungu: “Njoo, twende kwa mwonaji.”^c Kwa maana mtu ambaye leo anaitwa nabii, zamani alitwa mwonaji.) 10 Ndipo Sauli akamwambia hivi mtumishi wake: “Ulilosema ni jema. Haya twende.” Basi wakaenda katika jiji alimokuwa yule mtu wa Mungu wa kweli.

11 Walipokuwa wakipanda kwenda jijini, walikutana na wasichana waliokuwa wakionda kuteka maji. Basi wakaauliza: “Je, mwonaji^d yuko katika jiji hili?” 12 Wakajibu: “Ndiyo. Hajafika mbali sana. Fanyeni haraka, kwa sababu

9:8 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 9

a 1Sa 10:2

b 1Sa 3:19

c 1Sa 9:19
2Sa 15:27
1Nya 9:22
1Nya 29:29

d 1Sa 9:19

Safu ya 2

a 1Sa 7:9
1Sa 16:5b 1Fa 3:2
1Nya 16:39
2Nya 1:3

c Yos 18:11

d 1Sa 10:1
1Sa 15:1e Zb 106:43, 44
Zb 107:19f 1Sa 10:24
1Sa 15:17
Mdo 13:21

g 1Sa 9:13, 24

amekuja jijini leo, kwa maana leo watu wanatoa dhahibu^a mahali pa juu.^b 13 Mara tu mtakapoingia jijini, mtamkuta kabla hajapanda kwenda mahali pa juu kula chakula. Watu hawatakula mpaaka atakapofika, kwa maana yeye ndiye anayebariki dhahibu. Baada ya kufanya hivyo, wale walioalikwa wana-weza kula. Basi pandeni sasa moja kwa moja, mtamkuta.” 14 Basi wakapanda kwenda jijini. Walipokuwa wakiingia katikati ya jiji, Samweli alikuwa akija kukutana nao akielekea mahali pa juu.

15 Siku iliyotangulia kabla ya Sauli kufika, Yehova alikuwa amemwambia* Samweli: 16 “Kesho wakati kama huu, nitatuma mtu kwako kutoka katika nchi ya Benjamini.^c Utamtia mafuta awe kiongozi juu ya watu wangu Waisraeli,^d naye atawaokoa watu wangu kutoka mikononi mwa Wafilisti. Kwa sababu nimeyaona mateso ya watu wangu, na kilio chao kimenifikia.”^e 17 Samweli alipomwona Sauli, Yehova akamwambia: “Huyu ndiye mtu niliyekwambia, ‘Yeye ndiye atakayewaongoza watu wangu.’”^{*f}

18 Kisha Sauli akamkaribia Samweli katikati ya lango na kumuuliza: “Tafadhali niambie, nyumba ya mwonaji iko wapi?” 19 Samweli akamjibu Sauli: “Mimi ndiye mwonaji. Panda utangulie mbele yangu mahali pa juu, nawe utakula pamoja nami leo.^g Asubuhi nitakuruhusu uende, nami nitakueleza mambo yote

9:15 *Tnn., “amefunua sikio la.” 9:17 *Au “atakayewazuia watu wangu wasipite mipaka.”

unayotaka kujua.* **20** Kuhusu wale punda waliopotea siku tatu zilizopita,^a usiwe na wasiwasi juu yao, kwa maana wamepatikana. Vitu vyote vye-nye kutamanika vya Israeli ni vya nani? Je, si vyako na vya nyumba yote ya baba yako?”^b

21 Ndipo Sauli akasema: “Je, mimi si Mbenjamini kutoka katika kabila dogo zaidi kati ya makabila ya Israeli,^c na je, familia yangu si familia ya chini kabisa kati ya familia zote za kabila la Benjamini? Basi kwa nini unaniambia hivyo?”

22 Kisha Samweli akamchukua Sauli na mtumishi wake, akawaleta katika ukumbi wa kulia chakula, akawapa mahali pa kuketi mbele ya watu walioalikwa wapatao 30. **23** Samweli akamwambia mpishi: “Kilete chakula nilichokupa na kukuambia, ‘Kiweke kando.’” **24** Basi mpishi akainua ule mguu na nyama iliyokuwa juu yake, akauweka mbele ya Sauli. Samweli akasema: “Kilichokuwa kimehifadhiwa kimewekwa mbele yako. Kula, kwa maana kilihifadhiwa kwa ajili yako katika karamu hii. Kwa sababu niliwaambia, ‘Nimewaalika wageni.’” Basi Sauli akala pamoja na Samweli siku hiyo. **25** Kisha wakashuka kutoka mahali pa juu^d na kwenda jijini, naye akaendelea kuzungumza na Sauli kwenye paa la nyumba. **26** Wakaamka mapema, na kulipopambazuka, Samweli akamwita Sauli kutoka paani akisema: “Jitayarisha, ili nikusindikize.” Basi Sauli akajitayarisha na yeye pamoja na Samweli wakato-

9:19 *Tnn., “mambo yote yaliyo moyoni mwako.”

SURA YA 9

a 1Sa 9:3

b 1Sa 8:5,19
1Sa 12:13

c Amu 20:46, 47

d 1Sa 9:13,19

Safu ya 2

a 1Sa 9:3,10

SURA YA 10

b 1Sa 16:13
2Fa 9:2, 3c 1Sa 9:16
Mdo 13:21d Kut 19:5
Kum 32:9

e Mwa 35:19

f 1Sa 9:3, 5

g Mwa 28:19, 22

h Hes 11:25

ka nje. **27** Walipokuwa waki-shuka kuelekea ukingoni mwa jiji, Samweli akamwambia Sauli: “Mwambie mtumishi^a atangulie mbele yetu,” basi akatangulia. “Lakini wewe, si mama tuli sasa, ili nikujulishe neno la Mungu.”

10 Ndipo Samweli akachukua chupa ya mafuta na kuyamimina juu ya kichwa cha Sauli.^b Akambusu na kusema: “Yehova amekutia mafuta uwe kiongozi^c juu ya urithi wake.^d **2** Tuta- kapoachana leo, utakuta wanaume wawili karibu na kaburi la Raheli^e katika eneo la Benjamini kule Selsa, nao watakwambia, ‘Punda ulioenda kutafuta wamepatikana, lakini sasa baba yako amesahau kuhusu punda hao^f naye ana wasiwasi juu yako. Anauliza, ‘Nitafanya nini kuhusu mwanangu?’” **3** Kutoka huko nenda mpaka kwenye mti mkubwa wa Tabori, na huko utakutana na wanau- me watatu wakipanda kwenda kwa Mungu wa kweli kule Betheli,^g mmoja akiwa amebeba wanambuzi watatu, mwingine akiwa amebeba mikate mitatu, na mwingine akiwa amebeba mtungi mkubwa wa divai. **4** Watakusalimu na kukupa mikate miwili, unap- swa kuchukua mikate hiyo. **5** Kisha utafika kwenye kilima cha Mungu wa kweli, mahali ambapo pana kambi ya kijeshi ya Wafilisti. Utakapofika jijini, utakutana na kikundi cha manabii wakishuka kutoka mahali pa juu, na kinanda na tari na filimbi na kinubi vitapigwa mbele yao huku wakitoa unabii. **6** Roho ya Yehova itakutia nguvu,^h utatoa

unabii pamoja nao, nawe utabadilishwa kuwa mtu tofauti.^a **7** Baada ya ishara hizo kutokea, fanya lolote unaloweza kufanya kwa mkono wako, kwa sababu Mungu wa kweli yuko pamoja nawe. **8** Kisha ushuke na kunitangulia kwenda Gilgali,^b nami nitakufuata huko ili nitoe dhahabu za kuteketezwa na dhahabu za ushirika. Unapaswa kungoja kwa siku saba mpaka nitakapofika. Halafu nitakujulisha jambo unalopaswa kufanya.”

9 Mara tu Sauli alipogeuka ili amwache Samweli, Mungu akaanza kuabadili moyo wake uwe kama wa mtu mwingine, na ishara hizo zote zikatimia siku hiyo. **10** Basi wakatoka hapo na kupanda kwenye kilima, na kikundi cha manabii kikakutana naye. Mara moja roho ya Mungu ikamtia nguvu,^c naye akaanza kutoa unabii^d kati yao. **11** Watu wote waliomjua awali walipomwona akitoa unabii pamoja na manabii, wakulizana: “Mwana wa Kishi amepatwa na nini? Je, Sauli pia ni mmoja wa manabii?” **12** Ndipo mtu fulani wa mahali hapo akasema: “Lakini baba yao ni nani?” Basi kuka-
na na msemu* huu: “Je, Sauli pia ni mmoja wa manabii?”^e

13 Alipomaliza kutoa unabii, akaenda mahali pa juu. **14** Baadaye ndugu ya baba ya Sauli akamuuliza Sauli na mtumishi wake: “Mlienda wapi?” Akajibu: “Kuwatafuta punda,^f lakini hatukuwapata, kwa hiyo tukaenda kwa Samweli.” **15** Ndugu ya baba ya Sauli akamuuliza: “Tafa-

SURA YA 10

a 1Sa 10:10

b 1Sa 7:15, 16
1Sa 11:14

c Amu 14:5, 6
1Sa 11:6
1Sa 16:13

d 1Sa 10:6
1Sa 19:23

e 1Sa 19:24

f 1Sa 9:3

Safu ya 2

a 1Sa 7:5

b Kut 13:14
Kum 4:34

c 1Sa 8:7
1Sa 12:12

d Yos 7:16-18
Mdo 1:24

e 1Sa 9:21

f Mdo 13:21

g Amu 1:1
Amu 20:18, 28
1Sa 23:2

h 1Sa 9:2

dhali niambie, Samweli alikuambia nini?” **16** Sauli akamjibu: “Alituambia kwamba tayari punda wamepatikana.” Lakini Sauli hakumwambia jambo ambalo Samweli alisema kuhusu ufalme.

17 Kisha Samweli akawaita watu ili wakusanyike mbele za Yehova huko Mispa,^a **18** aka-
waambia Waisraeli: “Yehova, Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Mimi ndiye niliyewatoa Waisraeli nchini Misri na kuwaokoa kutoka mikononi mwa Misri^b na kutoka mikononi mwa falme zote zilizokuwa zikiwakandamiza. **19** Lakini leo mmemkataa Mungu wenu^c aliyekuwa Mwokozi wenu aliyewaokoa kutoka katika maovu yenu yote na taabu zenu, nanyi mlisema: ‘Hatutaki, unapaswa kumweka mfalme atutawale.’ Sasa simame-
ni mbele za Yehova kulingana na makabila yenu na kulingana na maelfu yenu.’”^{*}

20 Basi Samweli akaagiza makabila yote ya Israeli yakaribie,^d na kabila la Benjamine likachaguliwa.^e **21** Kisha akaagiza kabila la Benjamine likaribie kulingana na koo zao, basi ukoo wa Wamatri ukachaguliwa. Mwishowe Sauli mwana wa Kishi akachaguliwa.^f Lakini walipoenda kumtafuta, hawakumpata. **22** Kwa hiyo wakamuuliza Yehova:^g “Je, mtu huyo tayari amefika hapa?” Yehova akajibu: “Ndiye yule pale, amejificha kati ya mizigo.” **23** Basi wakambi-
mbia na kumleta kutoka mahali hapo. Aliposimama kati-
kati ya watu, alikuwa mrefu kuliko watu wote nao walimfika mabegani.^h **24** Samweli

10:19 *Au “koo zenu.”

10:12 *Yaani, methali.

akawaambia watu wote: “Je, mnamwona yule ambaye Yehova amemchagua,^a kwamba hakuna yeyote aliye kama yeye kati ya watu wote?” Basi watu wote wakaanza kupiga kelele wakisema: “Mfalme na aishi muda mrefu!”

25 Samweli akawaambia watu kuhusu haki za wafalme^b na kuziandika katika kitabu na kukiweka mbele za Yehova. Kisha Samweli akawaruhusu watu wote waende zao, kila mtu akaenda nyumbani kwake. **26** Sauli pia akaenda nyumbani kwake kule Gibeaa, akiwa pamoja na mashujaa ambao Yehova alikuwa amegusa mioyo yao. **27** Lakini wahuni fulani wakasema: “Huyu atatuokoaje?”^c Kwa hiyo wakamdharau, nao hawakumletea zawadi yoyote.^d Lakini hakusema jambo lolote kuhusu hilo.*

11 Nahashi Mwamoni^e akapanda na kupiga kambi ili kushambulia Yabeshi^f kule Gileadi. Watu wote wa Yabeshi wakamwambia Nahashi: “Fanya agano* pamoja nasi, nasi tutakutumikia.” **2** Nahashi Mwamoni akawaambia: “Nitafanya agano pamoja nanyi kwa sharti hili: macho yenu yote ya kulia yang’olewe. Nitafanya hivyo ili kuwaabisha Waisraeli wote.” **3** Wazee wa Yabeshi wakamwambia: “Tupe muda wa siku saba ili tuwatume wajumbe katika eneo lote la Israeli. Na ikiwa hakuna yeyote wa kutuokoa, tutajisalimisha kwako.” **4** Baada ya muda, wajumbe hao wakafika katika jiji la Gibeaa^g la Sauli na kuwaambia

10:27 * Tnn., “Naye alikuwa kama bubu.”
11:1 * Au “makubaliano.”

SURA YA 10

a Kum 17:14, 15
1Sa 9:17

b 1Sa 8:11-18

c 1Sa 11:12

d 1Fa 10:1, 10
2Nya 17:5

SURA YA 11

e Kum 2:19

f Amu 21:8
1Sa 31:11, 12

g 1Sa 10:26
1Sa 14:2

Safu ya 2

a Amu 3:9, 10
Amu 6:34
Amu 11:29
Amu 14:5, 6
1Sa 10:10, 11
1Sa 16:13

b 1Sa 11:3

c 1Sa 11:1

watu wote maneno hayo, na watu wote wakalia kwa sauti kubwa sana.

5 Lakini Sauli alikuwa aki-toka shambani akiwa nyuma ya mifugo yake, naye akauliza: “Watu wana shida gani? Kwa nini wanalia?” Basi wakamwambia maneno yaliyosemwa na watu wa Yabeshi. **6** Roho ya Mungu ikamtia nguvu Sauli^a alipoyasikia maneno hayo, akawaka hasira. **7** Kwa hiyo akachukua ng’ombe dume wawili, akawakata vipandevipande, akawatuma wajumbe wavipeleke katika eneo lote la Israeli wakisema: “Mtu yeyote ambaye hamfuati Sauli na Samweli ajue kwamba ng’ombe wake watafanyiwa hivi!” Na watu wakashikwa na hofu ya Yehova hivi kwamba wakatoka wote pamoja.* **8** Kisha akawahesabu kule Bezeki, Waisraeli walikuwa 300,000 na watu wa Yuda walikuwa 30,000. **9** Kwa hiyo wakawaambia wajumbe waliokuwa wamekuja: “Hivi ndivyo mnavyopaswa kuwaambia watu wa Yabeshi kule Gileadi, ‘Kesho wakati wa jua kali mtaokolewa.’” Basi wale wajumbe wakaja na kuwaambia watu wa Yabeshi, nao wakashangilia sana. **10** Ndipo watu wa Yabeshi wakasema: “Kesho tutajisalimisha kwenu, nanyi mtatutendea mpendavyo.”^b

11 Siku iliyofuata, Sauli aliwagawa watu katika vikosi vitatu, nao wakaingia katikati ya kambi wakati wa kesho la alfajiri* na kuwaua Waamoni^c mpaka jua lilipokuwa

11:7 * Tnn., “kama mtu mmoja.” 11:11 * Yaani, kuanzia saa 8 hivi usiku hadi saa 12 asubuhi.

kali. Watu waliookoka walitawanywa hivi kwamba hakuna watu wawili waliobaki pamoja. **12** Kisha watu wakamwambia Samweli: “Ni nani waliokuwa wakiuliza, ‘Je, Sauli atakuwa mfalme wetu?’^a Waleteni watu hao ili tuwaue.” **13** Hata hivyo, Sauli akasema: “Hakuna mtu yeyote anayepaswa kuuawa leo,^b kwa maana leo Yehova amewaokoa Waisraeli.”

14 Baadaye Samweli akawaambia watu: “Njooi twnde Gilgali^c tukamtangaze tena mfalme.”^d **15** Basi watu wote wakaenda Gilgali, na huko Gilgali wakamweka Sauli kuwa mfalme mbele za Yehova. Kisha wakatoa huko dhabihu za ushirika mbele za Yehova,^e na Sauli na watu wote wa Israeli wakasherehekea kwa shangwe kubwa.^f

12 Hatimaye Samweli akawaambia hivi Waisraeli wote: “Tazameni nimefanya* mambo yote mliyoomba nifanye, nami nimemweka mfalme awatawale.^g **2** Sasa huonydiye mfalme anayewaongoza ninyi!^h Lakini mimi ni mzee mwenye mvi, na wangu wako hapa pamoja nanyi,ⁱ nami nimewaongoza tangu nilipokuwa kijana mpaka leo hii.^j **3** Niko mbele yenu. Toeni ushahidi dhidi yangu mbele za Yehova na mbele ya mtiwamafuta wake:^k Nimechukua ng’ombe dume wa nani au punda wa nani?^l Au nimemlaghai nani au kumkandamiza nani? Nimepokea rushwa kutoka kwa nani ili nipotoshe haki?^m Ikiwa nimefanya hivyo, nita-

12:1 *Tnn., “nimesikiliza sauti yenu kuhusiana na.” 12:2 *Tnn., “anayete-mbea mbele yenu.” 12:3 *Tnn., “ili inifanye nitazame upande mwingine.”

SURA YA 11

a 1Sa 10:26, 27

b 2Sa 19:22

c 1Sa 7:15, 16

d 1Sa 10:17, 24

e Law 7:11

f 1Fa 1:39, 40
2Fa 11:12, 14
1Nya 12:39, 40

SURA YA 12

g 1Sa 8:5

1Sa 10:24
1Sa 11:14, 15

h 1Sa 8:20

i 1Sa 8:1, 3

j 1Sa 3:19

k 1Sa 9:16, 17
1Sa 10:1

l Hes 16:15

m Kum 16:19

Safu ya 2

a Kut 22:4
Law 6:4

b Kut 6:26

c Mwa 46:6

d Kut 2:23

e Kut 3:9, 10

f Yos 11:23

g Kum 32:18, 30
Amu 2:12, 14

h Amu 4:2

i Amu 10:7
Amu 13:1

j Amu 3:12

k Amu 2:18
Amu 3:9

l Amu 10:10, 15

m Amu 3:7

n Amu 2:13

o Amu 6:32

p Amu 11:1

q Ebr 11:32

warudishia.”^a **4** Nao wakasema: “Hujatulaghai wala kutukandamiza wala kupokea kitu chochote kile kutoka mkononi mwa yeyote.” **5** Basi akawaambia: “Yehova ni shahidi dhidi yenu, na mtiwamafuta wake ni shahidi leo kwamba hamkupata shtaka lolote dhidi yangu.”* Nao wakasema: “Yeye ni shahidi.”

6 Basi Samweli akawaambia watu: “Yehova, aliyemtumia Musa na Haruni na ambaye aliwatoa mababu zenu nchini Misri,^b ni shahidi. **7** Sasa simameni mahali penu, nami nitawahukumu mbele za Yehova kwa msingi wa matendo yote ya uadilifu ambayo Yehova amewatendea ninyi na mababu zenu.

8 “Baada tu ya Yakobo kuingia Misri^c na mababu zenu kuanza kumlilia Yehova awasaidie,^d Yehova alituma Musa^e na Haruni ili wawaongoze mababu zenu kutoka Misri na kuwawezesha kuishi mahali hapa.^f **9** Lakini walimsahau Yehova Mungu wao, naye akawauza^g mikononi mwa Siserah^h mkuu wa jeshi la Hasori na mikononi mwa Wafilistiⁱ na mikononi mwa mfalme wa Moabu,^j na maadui hao wakapigana nao. **10** Nao wakamlilia Yehova awasaidie^k na kusema, ‘Tumetenda dhambi,^l kwa maana tumekuacha wewe, Yehova, ili kuabudu Mabaa-ali^m na sanamu za Ashtorethi;ⁿ sasa tuokoe kutoka mikononi mwa maadui wetu ili tukutumikie.’ **11** Ndipo Yehova akamtuma Yerubaali^o na Bedani na Yeftha^p na Samweli,^q naye

12:5 *Tnn., “hamkupata chochote mkononi mwangu.”

akawaokoa ninyi kutoka mikononi mwa maadui waliowazunguka, ili mwishi kwa usalama.^a **12** Mlipoona kwamba Nahashi,^b mfalme wa Waamoni amekuja kuwashambulia, mliniambia tena na tena, 'Hatutaki, tumeazimia kuwa na mfalme wa kututawala!'^c hata ingawa Yehova Mungu wenu ndiye Mfalme wenu.^d **13** Sasa huyniye mfalme mliyemchagua, mliyeomba. Tazameni! Yehova amemweka mfalme awatawale.^e **14** Mkimwogopa Yehova^f na kumtumikia^g na kuitii sauti yake^h na msipoasi agizo la Yehova, na ikiwa ninyi pamoja na mfalme anayewatawala mtamfuata Yehova Mungu wenu, itakuwa vyema. **15** Lakini msipotii sauti ya Yehova na mkiasi agizo la Yehova, mkono wa Yehova utawashambulia ninyi na baba zenu.ⁱ **16** Sasa simameni mahali penu mwone jambo hili kubwa ambalo Yehova anatenda mbele ya macho yenu. **17** Je, huu si wakati wa kuvuna ngano? Nitamwomba Yehova alete ngurumo na mvua; ndipo mtakapojua na kuelewa uovu mkubwa mliofanya machoni pa Yehova kwa kuomba mfalme awatawale."^j

18 Basi Samweli akamwomba Yehova, naye Yehova akaleta ngurumo na mvua siku hiyo, hivi kwamba watu wote wakamwogopa sana Yehova na pia Samweli. **19** Na watu wote wakamwambia Samweli: "Sali kwa Yehova Mungu wako kwa ajili ya watumishi wako,^k kwa maana hatutaki kufa, kwa sababu tumeongeza uovu mwingine juu ya dhambi zetu zote kwa kuomba tupewe mfalme."

SURA YA 12

- a Law 26:6
b 1Sa 11:1
c 1Sa 8:5, 19
d Amu 8:23
1Sa 8:7
Isa 33:22
e 1Sa 9:16, 17
1Sa 10:24
f Kum 10:12
Kum 17:19
g Yos 24:14
h Kum 13:4
Kum 28:2
i Law 26:14, 17
Kum 28:15
Yos 24:20
j 1Sa 8:7
Ho 13:11
k 1Sa 7:5
1Sa 12:23

Safu ya 2

- a Kum 31:29
Yos 23:6
1Sa 12:15
b Kum 6:5
c Kum 32:21
Yer 2:11
d Zb 115:4, 5
Yer 16:19
e Yos 7:9
Zb 23:3
Zb 106:8
Yer 14:21
Eze 20:14
f 1Fa 6:13
Zb 94:14
Ro 11:1
g Kut 19:5
Kum 7:7
h 1Sa 12:14
Zb 111:10
Mhu 12:13
i Kum 10:12, 21
j Kum 28:15, 36
Yos 24:20

SURA YA 13

- k Mdo 13:21
l 1Sa 18:1
2Sa 1:4
2Sa 21:7
m Yos 18:28
1Sa 10:26
n Yos 13:2, 3
1Sa 9:16
o Yos 21:8, 17

20 Basi Samweli akawaambia watu: "Msiogope. Kwa kweli mmetenda uovu huu wote. Ila tu msigeuke na kuacha kumfuata Yehova,^a mtumikieni Yehova kwa moyo wenu wote.^b **21** Msigeuke na kufuata vitu vya ubatili,^{*c} ambavyo havina faida yoyote^d na ambavyo haviwezi kuokoa, kwa sababu ni vitu vya ubatili.^{*e} **22** Kwa ajili ya jina lake kuu,^e Yehova hatawaacha watu wake,^f kwa sababu Yehova ameamua mwenyewe kuwafanya ninyi kuwa watu wake.^g **23** Lakini mimi, siwezi kamwe kuwazia kumtendea Yehova dhambi kwa kuacha kusali kwa ajili yenu, nami nitaelelea kuwafundisha njia iliyo njema na iliyo sawa. **24** Ila tu mwogopeni Yehova,^h mtumikieni kwa uaminifu^{*} kwa moyo wenu wote, kwa maana angalieni mambo makuu aliyowatendea.ⁱ **25** Lakini mkifanya uovu bila kujali, ninyi pamoja na mfalme wenu mtafagiliwa mbali."^j

13 Sauli alikuwa na umri wa miaka . . .^{*} alipowekwa kuwa mfalme,^k na kwa miaka miwili alitawala Israeli. **2** Sauli alichagua wanauume 3,000 katika Israeli; 2,000 kati yao walikuwa pamoja na Sauli kule Mikmashi na katika eneo lenye milima la Betheli, na 1,000 walikuwa pamoja na Yonathani^l katika jiji la Gibeath^m la Benjamini. Aliwaruhusu waliobaki waende zao, kila mmoja kwenye hema lake. **3** Kisha Yonathani akaishambulia kambi ya kijeshi ya Wafilistiⁿ iliyokuwa Geba,^o na Wafilisti

12:21 *Au "vya kuwaziwa." 12:24 *Au "kwa unyoofu." 13:1 *Hati ya Kiebrania haionyeshi idadi ya miaka yake.

wakasikia habari hizo. Basi Sauli akaagiza pembe* ipigwe^a nchini kote, akisema: “Waebrania na wasikie!” **4** Waisraeli wote wakasikia habari hizi: “Sauli ameishambulia kambi ya kijeshi ya Wafilisti, na sasa Waisraeli wananuka mbele ya Wafilisti.” Basi watu wakakusanywa ili wamfuate Sauli huko Gilgali.^b

5 Wafilisti pia wakakusanyika pamoja ili wapigane na Waisraeli, nao walikuwa na magari 30,000 ya vita na wapanda farasi 6,000 na wanajeshi wengi kama chembe za mchanga kwenye ufuu wa baharini;^c nao wakapanda na kupiga kambi kule Mikmashi upande wa mashariki wa Beth-aveni.^d

6 Na wanaume wa Israeli wakaona kwamba walikuwa hatarini, kwa sababu watu walikuwa chini ya mkazo mkali; basi watu wakajificha ndani ya mapango,^e mashimo, miamba, mahandaki, na hifadhi za maji.

7 Hata baadhi ya Waebrania walivuka Yordani na kuingia nchi ya Gadi na Gileadi.^f Lakini Sauli alikuwa bado Gilgali, na watu wote waliomfuata walikuwa wakitetemeka. **8** Aliendelea kungoja kwa siku saba mpaka wakati uliowekwa na Samweli ulipofika, lakini Samweli hakuja Gilgali, na watu walikuwa wakitawanyika kutoa kwake. **9** Mwishowe Sauli akasema: “Nileteeni dhahihu ya kuteketezwa na dhahihu za ushirika.” Basi akaitoa dhahihu ya kuteketezwa.^g

10 Lakini mara tu alipomaliza kutoa dhahihu ya kutekelezwa, Samweli akafika. Kwa hiyo Sauli akaenda kumpo-

SURA YA 13

a Amu 3:26, 27
Amu 6:34
2Sa 2:28

b Yos 5:9
1Sa 11:14

c Kum 20:1

d Yos 7:2
Yos 18:11, 12
1Sa 14:23

e 1Sa 14:11

f Hes 32:1, 33
Yos 13:24, 25

g 1Sa 15:22, 23

Safu ya 2

a 1Sa 13:6, 8

b 1Sa 13:5

c 1Sa 15:11

d 1Sa 15:28

e 1Sa 16:1
2Sa 7:15
Zb 78:70
Mdo 13:22

f Mwa 49:10
2Sa 5:2
2Sa 7:8
1Nya 28:4

g Met 11:2

h 1Sa 13:7
1Sa 14:2

i 1Sa 13:3

j 1Sa 13:2

kea na kumbariki. **11** Kisha Samweli akamuuliza: “Umfanya nini?” Sauli akamjibu: “Niliona kwamba watu wanatawanyika kutoka kwangu,^a nawe hukuja kwa wakati uliowekwa, na Wafilisti walikuwa wakikusanyika huko Mikmashi.^b **12** Kwa hiyo nikajiambia, ‘Sasa Wafilisti watashuka kunishambulia Gilgali, nami sijatafuta kibali cha* Yehova.’ Kwa hiyo nikahisi kwamba nina wajibu wa kutoa dhahihu ya kuteketezwa.”

13 Ndipo Samweli akamwambia Sauli: “Umetenda kipumbavu. Hukutii amri ambayo Yehova Mungu wako alikupa.^c Kama ungetii, Yehova angeimarisha ufalme wako juu ya Waisraeli milele. **14** Lakini sasa ufalme wako hautadumu.^d Yehova atamtafuta mtu anayeupendeza moyo wake,^e na Yehova atamweka kuwa kiongozi juu ya watu wake,^f kwa sababu hukutii mambo uliyoamriwa na Yehova.”^g

15 Kisha Samweli akainuka na kupanda kwenda zake kutoka Gilgali mpaka jiji la Gibeala Benjaminini, naye Sauli akawahesabu watu; wale waliobaki naye walikuwa wanaume wapatao 600.^h **16** Sauli na Yonathani mwana wake pamoja na watu waliobaki pamoja nao walikuwa wakikaa katika jiji la Gebaⁱ la Benjaminini, nao Wafilisti walikuwa wamepiga kambi kule Mikmashi.^j **17** Na makundi ya wavamizi yalikuwa yakitoka katika kambi ya Wafilisti katika vikosi vitatu. Kikosi kimoja kilikuwa kikielekea kwenye barabara inayoenda Ofra, katika nchi

13:3 *Au “tarumbeta.”

13:12 *Au “sijautuliza uso wa.”

ya Shuali; **18** kikosi kingine kilikuwa kikielekea kwenye barabara ya Beth-horoni;^a na kikosi cha tatu kilikuwa kifikuata barabara inayoelekea kwenye mpaka ulio ng'ambo ya bonde la Seboimu, kuelekea nyikani.

19 Basi hakukuwa na fundi yeyote wa chuma katika nchi yote ya Israeli, kwa sababu Wafilisti walikuwa wamesema: "Ili Waebrania wasitengeze upanga wala mkuki." **20** Na Waisraeli wote walilazimika kushuka kwenda kwa Wafilisti ili majembe yao ya plau, sururu, mashoka, au miundu yao inolewe. **21** Bei ya kunoa ilikuwa pimu moja* kwa majembe ya plau, kwa sururu, kwa vifaa vyenye meno matatu, kwa mashoka, na pia kwa ajili ya kurekebisha mchokoo wa ng'ombe. **22** Na siku ya vita, hakuna yeyote kati ya watu waliokuwa pamoja na Sauli na Yonathani aliyekuwa na upanga wala mkuki mkononi mwake;^b Sauli na Yonathani mwanawe ndio tu waliokuwa na silaha.

23 Basi kikosi cha wanajeshi* Wafilisti kilikuwa kimeenda kwenye kivuko kilicho kwenye njia inayoenda Mikmashi.^c

14 Siku moja Yonathani^d mwana wa Sauli alimwambia hivi mtumishi aliyembebea silaha: "Njoo tuvuke, twende kwenye kituo cha ulinzi cha Wafilisti upande wa pili." Lakini hakumwambia baba yake jambo hilo. **2** Sauli alikuwa akikaa kari-

13:21 *Kipimo cha zamani ambacho ni karibu theluthi mbili za shekeli. 13:23 *Tnn., "kituo cha ulinzi cha."

SURA YA 13

a Yos 10:11

b 1Sa 17:47, 50

c 1Sa 13:2
1Sa 14:4, 5

SURA YA 14

d 1Sa 14:49

1Sa 18:1

2Sa 1:4

Safu ya 2

a 1Sa 10:26

b 1Sa 13:15

c 1Sa 22:9

d 1Sa 4:21

e 1Sa 2:12
1Sa 4:17

f 1Sa 1:9

g Yos 18:1
1Sa 1:3h Kut 29:5
Hes 27:21

i 1Sa 13:2, 3

j Mwa 17:9, 10
Amu 14:3
Amu 15:18
1Sa 17:36
1Nya 10:4k Amu 7:2
2Fa 6:15, 16
2Nya 14:11

bu na jiji la Gibea^a chini ya mkomamanga kule Migroni, na wanaume wapatao 600 walikuwa pamoja naye.^b **3** (Na Ahiya mwana wa Ahitubu,^c ndugu ya Ikabodi,^d mwana wa Finehasi,^e mwana wa Eli,^f kuhani wa Yehova kule Shilo,^g alikuwa amebeba efodi.)^h Na watu hawakujua kwamba Yonathani alikuwa ameondoka. **4** Basi kati wa njia ambazo Yonathani alijaribu kutumia kuvuka ili afike kwenye kituo cha ulinzi cha Wafilisti, kulikuwa na mwamba ulio na umbo la jino upande huu na mwamba mwingine ulio na umbo la jino upande wa pili; mwamba mmoja uliitwa Bose-si, na mwamba wa pili uliitwa Sene. **5** Mwamba mmoja ulikuwa nguzo upande wa kaskazini ng'ambo ya Mikmashi, na wa pili ulikuwa upande wa kusini ng'ambo ya Geba.ⁱ

6 Basi Yonathani akamwambia mtumishi wake aliyembebea silaha: "Njoo tuvuke na kwenda kwenye kituo cha ulinzi cha wanaume hawa wasiotahiriwa.^j Labda Yehova atatusaidia, kwa maana hakuna kitu chochote kinachoweza kumzuia Yehova kuokoa kwa kutumia watu wengi au wachache."^k **7** Ndipo mtumishi wake aliyembebea silaha akamwambia: "Fanya jambo lolote ambalo moyo wako unakuchochea kufanya. Nenda popote unapotaka, nami nitaifuata popote ambapo moyo wako unakuchochea kwenda." **8** Ndipo Yonathani akasema: "Tutavuka kwa wanaume wale ili watuone. **9** Wakituaambia, 'Simameni papo hapo mpaka tuje mlipo!' basi tutasimama papo hapo, hatutapa-

nda kwenda walipo. **10** Lakin wakisema, 'Njooi hapa juu tupambane!' tutapanda, kwa sababu Yehova atawatia mikononi mwetu. Hiyo ndiyo itakayokuwa ishara yetu."^a

11 Basi wote wawili wakajitokeza mbele ya kituo cha ulinzi cha Wafilisti. Wafilisti wakasema: "Tazameni! Waebrania wanatoka katika mashimo walimokuwa wamejificha."^b

12 Kwa hiyo wanaume waliokuwa kwenye kituo hicho cha ulinzi wakamwambia Yonathani na mtumishi wake aliyembebea silaha: "Njooi hapa juu tulipo, nasi tutawafunza somo!"^c Mara moja Yonathani akamwambia hivi mtumishi aliyembebea silaha: "Nifuate, kwa kuwa Yehova atawatia mikononi mwa Waisraeli."^d

13 Basi Yonathani akapanda kwa mikono na miguu yake, na mtumishi wake aliyembebea silaha alikuwa nyuma yake; na Yonathani akaanza kuwashambulia na kuwaangusha Wafilisti, na mtumishi wake aliyembebea silaha alikuwa akiwaua nyuma ya Yonathani.

14 Katika shambulizi la kwanza la Yonathani na mtumishi aliyembebea silaha, waliwaua wanaume wapatao 20 katika shamba lenye ukubwa wa karibu nusu eka linaloweza kulimwa kwa plau.*

15 Ndipo hofu ikaenea katika kambi iliyo shambani na miongoni mwa watu wote waliokuwa katika kituo cha ulinzi, na hata makundi ya wavamizi^e yakashikwa na hofu. Dunia ikaanza kutetemeka, kukawa na hofu kubwa kutoka

14:14 *Yaani, eneo linaloweza kulimwa kwa plau na ng'ombe dume wawili katika siku moja.

SURA YA 14

a Mwa 24:14
Amu 7:11
1Sa 10:7

b 1Sa 13:6
1Sa 14:22

c 1Sa 14:10

d 1Sa 14:6
2Sa 5:23, 24
2Fa 6:15, 16

e 1Sa 13:17

Safu ya 2

a 1Sa 10:26
1Sa 14:2

b 1Sa 14:20

c 1Sa 14:3

d 1Sa 13:6

e Kum 33:29
Amu 2:18

f 1Sa 13:5

kwa Mungu. **16** Walinzi wa Sauli waliokuwa katika jiji la Gibeaa la Benjamini wakao-na kwamba machafuko yalikuwa yakienea kila upande.^b

17 Sauli akawaambia watu waliokuwa pamoja naye: "Tafadhali, wahesabuni watu, mwone ni nani aliyetuacha." Walipohesabu, wakagundua kwamba Yonathani na mtumishi wake aliyembebea silaha hawakuwepo. **18** Basi Sauli akamwambia Ahiya:^c "Lilete karibu Sanduku la Mungu wa kweli!" (Kwa maana wakati huo* Sanduku la Mungu wa kweli lilikuwa pamoja na Waisraeli.) **19** Sauli alipokuwa akiongea na kuhani, machafuko yaliyokuwa katika kambi ya Wafilisti yalizidi kuongezeka. Ndipo Sauli akamwambia hivi kuhani: "Acha unachofanya."*

20 Kwa hiyo Sauli na watu wote waliokuwa pamoja naye wakakusanyika na kwenda vitani, na huko wakapata kwamba Wafilisti walikuwa wamshambuliana wenyewe kwa wenyewe kwa mapanga yao, na machafuko yalikuwa makubwa sana. **21** Pia, Waebrania ambao awali waliwaunga mkono Wafilisti na walioingia pamoja nao kambini walienda kujiunga na Waisraeli chini ya usimamizi wa Sauli na Yonathani. **22** Wanaume wote wa Israeli waliokuwa wamejificha^d katika eneo lenye milima la Efraimu wakasikia kwamba Wafilisti wamekimbia, nao pia wakaingia vitani na kuwafuata. **23** Basi Yehova akawao-koa Waisraeli siku hiyo,^e na vita vikaenea mpaka Bethaveni.^f

14:18 *Tnn., "siku hiyo." **14:19** *Tnn., "Rudisha mkono wako."

24 Lakini wanaume wa Israeli walikuwa chini ya mka-zo mkali siku hiyo, kwa kuwa Sauli alikuwa amewaapisha hivi: "Alaaniwe mtu yeyote atakayekula chakula chochote* kabla ya jioni na kabla sijalipiza kisasi dhidi ya maadui wangu!" Kwa hiyo hakuna yeyote miongoni mwa aliyekula chakula chochote.^a

25 Basi watu wote wakafika* msituni, na kulikuwa na asali ardhini. **26** Watu wali-poingia msituni, waliona asali ikidondoka, lakini hakuna yeyote aliyethubutu kunyoosha mkono wake ili kuila, kwa sababu waliogopa kile kiapo. **27** Lakini Yonathani hakumsikia baba yake akiwaapisha watu,^b kwa hiyo akanyoosha ncha ya fimbo iliyokuwa mkononi mwake na kuichovya ndani ya sega la asali. Alipourudisha mkono wake kinywani na kuila, macho yake yakang'aa. **28** Ndipo mtu mmoja akasema: "Baba yako aliwaapisha watu vikali akisema, 'Na alaaniwe mtu atakayekula chakula leo!'^c Ndio sababu watu wamechoka sana." **29** Hata hivyo, Yonathani akasema: "Baba yangu ameleta shida kubwa nchini. Angalieni jinsi macho yangu yalivyong'aa nilipoonja asali hii kidogo. **30** Hali ingekuwa bora zaidi ikiwa watu wangekula kwa uhuru^d leo baadhi ya nyara walizopata kutoka kwa maadui wao! Kwa maana Wafilisti wengi hata zaidi wanguewa." **31** Siku hiyo, waliendelea kuwaua Wafilisti kuanzia Mikmashi mpaka Aiyaloni,^e na watu wakachoka sana.

14:24 *Tnn., "mkate wowote." 14:25 *Tnn., "nchi yote ikafika."

SURA YA 14

a Law 5:4
Hes 30:2
Kum 23:21

b 1Sa 14:17

c 1Sa 14:24

d 1Sa 14:26

e Yos 10:12

Safu ya 2

a Mwa 9:4
Law 3:17
Law 17:10
Kum 12:16
Mdo 15:29

b Kum 12:23

c 1Sa 14:32

d 1Sa 7:15, 17

e Hes 27:21
1Sa 30:7, 8

f Amu 1:1
1Sa 30:8
2Sa 5:19

32 Basi watu wakaanza kuki-mbililia nyara kwa pupa, wakachukua kondoo na ng'ombe na ndama na kuwachinjia ardhini, nao wakala nyama pamoja na damu.^a **33** Basi Sauli akaambiwa hivi: "Tazama! Watu wanamtendea Yehova dhambi kwa kula nyama pamoja na damu."^b Ndipo akasema: "Mmetenda kwa ukosefu wa imani. Bingirisheni jiwe kubwa juu yangu mara moja." **34** Kisha Sauli akasema: "Nendeni kotekote miongoni mwa watu mkawaambie, 'Ni lazima kila mmoja wenu aje na ng'ombe dume wake na kondoo wake mwachinjie hapa na kuwala. Msimtendea Yehova dhambi kwa kula nyama pamoja na damu.'"^c Basi kila mmoja wao akaja na ng'ombe dume wake usiku huo na kumchinja mahali hapo. **35** Na Sauli akamjengea Yehova madhabahu.^d Hiyo ndiyo iliyokuwa madhabahu ya kwanza aliyomjengea Yehova.

36 Baadaye Sauli akasema: "Acheni tushuke tuwafuatie Wafilisti usiku na kuwaporu mpaka asubuhi wakati wa mapambazuko. Hatutamwacha hai mtu yeyote." Basi wakasema: "Fanya jambo lolote unalona ni jema." Kisha kuhani akasema: "Na tumkaribie Mungu wa kweli mahali hapa."^e **37** Naye Sauli akamuuliza Mungu: "Je, nishuke nikawafuatie Wafilisti?^f Je, utawatia mikononi mwa Waisraeli?" Lakini Mungu hakumjibu siku hiyo. **38** Basi Sauli akasema: "Njoo-ni hapa, enyi wakuu wote wa watu, mtafute ni dhambi gani iliyotendwa leo. **39** Kwa haka kama anavyoishi Yehova, aliyewaokoa Waisraeli,

hata kama ni mwanangu Yonathani, ni lazima afe." Lakini hakuna mtu yeyote aliyemjibu. **40** Kisha akawaambia Waisraeli wote: "Mtakuwa upande mmoja, na mimi na mwanangu Yonathani tutakuwa upande wa pili." Ndipo watu wakamwambia Sauli: "Fanya jambo lolote unaloona ni jema."

41 Kisha Sauli akamwambia Yehova: "Ee Mungu wa Israeli, jibu kwa Thumimu!"^a Ndipo Yonathani na Sauli wakachaguliwa, nao watu wakawa huru. **42** Basi Sauli akasema: "Pigeni kura^b kuamua kati yangu na mwanangu Yonathani." Kisha Yonathani akachaguliwa. **43** Halafu Sauli akamuuliza Yonathani: "Niambie, umefanya nini?" Yonathani akamwambia: "Nilionja tu asali kidogo kwa ncha ya fimbo iliyo mikononi mwangu.^c Nipo hapa! Niko tayari kufal!"

44 Basi Sauli akasema: "Mungu na akuadhibu, tena vikali, ikiwa hutakufa, Yonathani."^d **45** Lakini watu wakamwambia Sauli: "Je, Yonathani afe, ambaye ameleta ushindi*^e huu mkubwa katika Israeli? Ni jambo lisiloweza kuwaziwa kamwe! Kwa hakika kama anavyoishi Yehova, hakuna unywele hata mmoja wa kichwa chake unaopaswa kuanguka ardhini, kwa maana alitenda pamoja na Mungu leo."^f Hivyo watu wakamwokea[#] Yonathani, naye hakufa.

46 Basi Sauli akaacha kuwafuatia Wafilisti, nao Wafilisti wakarudi katika eneo lao.

47 Sauli akauimarisha ufalme wake juu ya Waisraeli,

14:45 *Au "wokovu." #Tnn., "wakamkomboa."

SURA YA 14

a Kut 28:30
Kum 33:8
Ezr 2:62, 63

b Met 16:33

c 1Sa 14:27

d 1Sa 14:24

e 1Sa 14:14

f 1Sa 14:6

Safu ya 2

a 1Sa 12:9

b 1Sa 11:11

c Mwa 36:8

d 2Sa 10:6

e 1Sa 9:16, 17

f Kut 17:14
Kum 25:19
1Sa 15:3

g 1Sa 31:2
1Nya 8:33
1Nya 9:39

h 1Sa 18:17

i 1Sa 18:27
1Sa 25:44
2Sa 3:13
2Sa 6:20

j 1Sa 17:55
2Sa 2:8
2Sa 3:27

k 1Sa 9:1

l 1Fa 2:5

m Mwa 49:27
1Sa 9:16, 17

n 1Sa 8:11
1Sa 10:26

SURA YA 15

o 1Sa 9:16
1Sa 10:1

p 1Sa 12:14

q Kut 17:8
Hes 24:20
Kum 25:17, 18

r Kut 17:14
Kum 25:19
1Nya 4:43

s Law 27:29
1Sa 15:18

t Kum 9:1, 3

akapigana na maadui wake wote waliomzunguka, alipigana na Wamoabu,^a Waamoni,^b Waedomu,^c wafalme wa Soba,^d na Wafilisti;^e na mahali popote alipoenda aliwashinda. **48** Alipigana kwa ushujaa na kuwashinda Waamaleki^f na kuwaokoa Waisraeli kutoka mikononi mwa waporaji.

49 Wana wa Sauli walikuwa Yonathani, Ishvi, na Malkishua.^g Na alikuwa na mabinti wawili; mkubwa aliitwa Merahu,^h na mdogo aliitwa Mikali.ⁱ **50** Mke wa Sauli aliitwa Ahinoamu binti ya Ahimaazi. Mkuu wa jeshi lake aliitwa Abneri^j mwana wa Neri, ndugu ya baba ya Sauli. **51** Kishi^k alikuwa baba ya Sauli, na Neri^l baba ya Abneri alikuwa mwana wa Abieli.

52 Kulikuwa na vita vikali dhidi ya Wafilisti siku zote za Sauli.^m Sauli alipomwona mwanamume yeyote mwenye nguvu au jasiri alimwandikisha katika utumishi wake.ⁿ

15 Kisha Samweli akamwambia Sauli: "Yehova alinituma nikitite mafuta uwe mfalme juu ya watu wake Waisraeli,^o sasa sikiliza anavyosema Yehova.^p **2** Yehova wa majeshi anasema hivi: 'Nitaoadhibu Waamaleki kwa sababu waliwapinga Waisraeli walipokuwa njiani wakipanda kutoka Misri.^q **3** Sasa, nenda uwashambulie Waamaleki^r na kuwaangamiza^s wao pamoja na vitu vyao vyote. Usiwaache hai;^{*} unapaswa kuwaua,^t wanaume na wana wake, watoto wadogo na wale wanaonyonya, ng'ombe dume na kondoo, ngamia na pia

15:3 *Au "Usiwahurumie."

punda.”^a **4** Sauli akawakusanya watu na kuwahesabu huko Telaimu: Kulikuwa na wanajeshi 200,000 wanaotembea kwa miguu na wanaume 10,000 wa Yuda.^b

5 Sauli akaenda mpaka kwenye jiji la Amaleki, akaanzia kando ya bonde. **6** Ndipo Sauli akawaambia hivi Wakeni: ^c“Nendeni, ondoke-ni kati ya Waamaleki ili nisi-wafagilie mbali pamoja nao.”^d Kwa maana mliwatendea watu wote wa Israeli^e kwa upe-ndo mshikamanifu walipotoka Misri.” Basi Wakeni wakaondoka kati ya Waamaleki. **7** Kisha Sauli akawaangamiza Waamaleki^f kuanzia Havi-la^g mpaka Shuri,^h jiji lililo karibu na Misri. **8** Akamkamata Agagiⁱ mfalme wa Amaleki akiwa hai, lakini watu wengine wote akawaangamiza kwa upanga.^j **9** Hata hivyo, Sauli na watu wake walimwacha hai* Agagi na kondoo walio bora, ng’ombe, wanyama waliononeshwa, kondoo dume, na vitu vyote vizuri.^k Hawakutaka kuviangamiza. Lakini waliangamiza vitu vyote visivyo na thamani na visivyofaa.

10 Basi neno la Yehova likamjia Samweli: **11** “Ninasi-kitika* kwamba nimemwaka Sauli kuwa mfalme, kwa sababu ameacha kunifuata naye hajatekeleza maneno yangu.”^l Samweli akakasirika sana, akaendelea kumlilia Yehova usiku kucha.^m **12** Samweli alipoamka asubuhi na mapema ili akutane na Sauli, aliambiwa hivi: “Sauli alienda Karmeli,ⁿ na huko akajisimamishia mnara wa uku-

15:9 *Au “walimhurumia.” 15:11 *Au “Ninahuzunika.”

SURA YA 15

a Kum 13:17
Yos 6:18

b 1Sa 11:8
1Sa 13:15

c Hes 10:29, 32
Hes 24:21
Amu 1:16

d Mwa 18:25
Mwa 19:12, 13
Yos 6:17

e Kut 18:9, 12

f Kum 25:19
1Sa 14:47, 48

g Mwa 25:17, 18

h 1Sa 27:8

i 1Sa 15:33

j Law 27:29
1Sa 15:3

k Yos 7:12

l 1Sa 13:13
1Sa 15:3

m 1Sa 16:1

n Yos 15:20, 55

Safu ya 2

a 2Sa 18:18

b 1Sa 15:3

c 1Sa 15:10, 11

d 1Sa 9:21
1Sa 10:22

e 1Sa 9:16
1Sa 10:1

f 1Sa 15:3

g Kum 25:19

h Kum 13:17
1Sa 15:9

i Law 27:29
Kum 7:16
1Sa 15:3, 9

mbusho.^a Kisha akageuka na kushuka mpaka Gilgali.” **13** Mwishowe Samweli alipomfikia Sauli, Sauli akamwambia: “Yehova na akubariki. Nimetekeleza neno la Yehova.” **14** Lakini Samweli akamwambia: “Basi mbona nasikia milio ya kondoo na ng’ombe?”^b **15** Sauli akamjibu: “Waliletwa kutoka kwa Waamaleki, kwa sababu watu waliwaacha hai* kondoo bora na ng’ombe bora ili wawatoe dhabihu kwa Yehova Mungu wako; lakini vitu vilivyobaki tuliviangamiza.” **16** Ndipo Samweli akamwambia Sauli: “Nyamaza! Acha nikwambie jambo ambalo Yehova aliniambia jana usiku.”^c Basi akamwambia: “Sema!”

17 Samweli akamwambia: “Je, hukujiona kuwa mtu asi-yefaa^d ulipowekwa kuwa kiongozi wa makabila ya Israeli na Yehova alipokutia mafuta kuwa mfalme wa Israeli?”^e **18** Baadaye Yehova alikupa kazi na kukuambia, ‘Nenda, uwaangamize Waamaleki hao watenda dhambi.’^f Pigana nao mpaka uwaangamize kabisa.’^g **19** Basi kwa nini hukuitii sauti ya Yehova? Badala yake, ulikimbilia nyara kwa pupa^h na kufanya maovu machoni pa Yehova!”

20 Hata hivyo, Sauli akamwambia Samweli: “Lakini nimeitii sauti ya Yehova! Nimefanya kazi ambayo Yehova alinituma nifanye, nikamleta Agagi mfalme wa Waamaleki na kuwaangamiza Waamaleki.ⁱ **21** Lakini watu walichukua kondoo na ng’ombe kutoka kwenye nyara, vitu bora

15:15 *Au “waliwahurumia.”

kati ya vitu vilivyopaswa kuangamizwa, ili wavitoe dhabihu kwa Yehova Mungu wako huko Gilgali.”^a

22 Ndipo Samweli akasema: “Je, Yehova hupendezwa zaidi na dhabihu za kuteketewa na dhabihu nyinginezo^b kuliko kuitii sauti ya Yehova? Tazama! Kutii ni bora kuliko dhabihu,^c na kusikiliza kuliko mafuta^d ya kondoo dume; **23** kwa maana uasi^e ni sawa na dhambi ya uaguzi,^{*f} na kutenda kwa kimbelebele ni sawa na kutumia nguvu za uchawi na ibada ya sanamu.”^g Kwa kuwa umelikataa neno la Yehova,^g yeye pia amekukataa usiwe mfalme.”^h

24 Ndipo Sauli akamwambia Samweli: “Nimetenda dhambi, kwa kuwa nimeasi agizo la Yehova na maneno yako, kwa sababu niliwaogopa watu na kusikiliza maneno yao. **25** Sasa, tafadhali, nisamehe dhambi yangu, nawe urudi pamoja nami ili nimwianamie Yehova.”ⁱ **26** Lakini Samweli akamwambia Sauli: “Sitarudi pamoja nawe, kwa kuwa umelikataa neno la Yehova, naye Yehova amekukataa usiendelee kuwa mfalme wa Israeli.”^j **27** Samweli alipokuwa akigeuka aende zake, Sauli akaushika upindo wa joho lake lisilo na mikono, lakini likararuka. **28** Ndipo Samweli akamwambia: “Yehova ameurarua ufalme wa Israeli kutoka kwako leo, naye atampa mwenzako aliyebora kuliko wewe.”^k **29** Ilastoshe, Mtukufu wa Israeli! hatasema uwongo^m wala kubadi-

15:23 *Au “ubashiri.” ^gTnn., “sanamu za terafimu,” yaani, miungu ya familia; sanamu.

SURA YA 15

a 1Sa 15:15

b Isa 1:11

c Met 21:3
Ho 6:6
Mk 12:33

d Law 3:16

e 1Sa 12:15

f Law 20:6
Kum 18:10, 12
1Nya 10:13

g 1Sa 15:3

h 1Sa 13:14
1Sa 16:1
Mdo 13:22

i 1Sa 15:30

j 1Sa 13:14
1Sa 16:1k 1Sa 13:14
1Sa 16:12, 13
Mdo 13:22

l 1Nya 29:11

m Tit 1:2
Ebr 6:18

Safu ya 2

a Hes 23:19

b 1Sa 15:25

c Kut 17:14
Kum 25:19
1Sa 15:3

d 1Sa 16:1

e 1Sa 15:11

SURA YA 16

f 1Sa 15:23, 26

g 1Sa 15:35

h 1Fa 1:39

li nia yake,^{*} kwa maana Yeye si mwanadamu abadili nia yake.”^g^a

30 Sauli akasema: “Nimetenda dhambi. Lakini tafadhali niheshimu mbele ya wazee wa watu wangu na mbele ya Waisraeli. Rudi pamoja nami, nami nitamwinamia Yehova Mungu wako.”^b **31** Basi Samweli akarudi pamoja na Sauli, na Sauli akamwinamia Yehova.

32 Kisha Samweli akasema: “Mleteni hapa Agagi mfalme wa Waamaleki.” Ndipo Agagi akaja kwake akisitasita,^{*} kwa sababu Agagi alisema moyoni mwake: “Kwa hakika hatari ya kifo imepita.”^g **33** Hata hivyo, Samweli akasema: “Kama upanga wako ulivyofanya wanawake wafiwe na watoto, ndivyo mama yako atakavyofiwa zaidi miongoni mwa wanawake.” Papo hapo Samweli akamkatakata Agagi vipandevipande mbele za Yehova huko Gilgali.^c

34 Kisha Samweli akaenda zake Rama, naye Sauli akapanda kwenda nyumbani kwake katika jiji la Gibe la Sauli.

35 Samweli hakumwona Sauli tena mpaka siku alipokufa, kwa maana Samweli alikuwa akimwombolezea Sauli.^d Yehova akaghairi kwamba alikuwa amemweka Sauli kuwa mfalme wa Israeli.^e

16 Mwishowe Yehova akamuuliza Samweli: “Kwa kuwa nitemkataa Sauli asitawale akiwa mfalme wa Israeli,^f utaendelea jumwombolezea mpaka lini?^g Jaza pembe yako mafuta,^h uende. Nitakutuma

15:29 *Au “hataghairi.” ^gAu “aghairi.”
15:32 *Au labda, “kwa ujasiri.” ^gTnn., “uchungu wa kifo umepita.”

kwa Yese^a Mbethlehemu, kwa sababu nimejichagulia mfalme kutoka miongoni mwa wanawe.”^b **2** Lakini Samweli akasema: “Nitaendaje? Sauli akisikia habari hii, ataniua.”^c Yehova akamwambia: “Nenda na ng’ombe mchanga, useme, ‘Nimekuja kumtolea Yehova dhabihu.’” **3** Mwalike Yese kwenye dhabihu; kisha nita-kujulisha utakalofanya. Utamtia mafuta kwa ajili yangu yule nitakayekuonyesha.”^d

4 Samweli alifanya mambo aliyoaambiwa na Yehova. Alipofika Bethlehemu,^e wazee wa jiji walitetemeka walipokutana naye, wakamuuliza: “Je, umekuja kwa amani?” **5** Akajibu: “Nimekuja kwa amani. Nimekuja kumtolea Yehova dhabihu. Jitakaseni, mje pamoja nami kwenye dhabihu.” Kisha akamtakasa Yese na wanawe, halafu akawaalika kwenye dhabihu. **6** Walipokuwa wakiingia, Samweli alimwona Eliabu^f na kusema: “Hakika mtiwa-mafuta wa Yehova amesimama hapa mbele zake.” **7** Lakini Yehova akamwambia Samweli: “Usitazame sura yake wala urefu wake,^g kwa maana nimemkataa. Kwa kuwa Mungu haoni kama mwanadamu anavyoona, kwa maana mwanadamu huona kinachoonekana kwa macho, lakini Yehova huona ndani ya moyo.”^h **8** Kisha Yese akamwita Abinadabu,ⁱ akampitisha mbele ya Samweli, lakini Samweli akasema: “Huyu pia Yehova hajamchagua.” **9** Kisha Yese akampitisha Shamma,^j lakini Samweli akasema: “Hata huyu Yehova hajamchagua.” **10** Basi Yese akawapitisha wanawe saba

SURA YA 16

a Ru 4:17
1Nya 2:12

b Mwa 49:10
1Sa 13:14
Zb 78:70
Mdo 13:22

c 1Sa 22:17

d Zb 89:20

e Ru 4:11
1Sa 20:6

f 1Sa 17:28
1Nya 2:13

g 1Sa 10:21, 23

h 1Fa 8:39
1Nya 28:9
Zb 7:9
Met 24:12
Yer 17:10
Mdo 1:24

i 1Sa 17:13
1Nya 2:13

j 2Sa 13:3

Safu ya 2

a 1Sa 17:14

b 2Sa 7:8
Zb 78:70

c 1Sa 17:42

d 1Sa 13:14
Zb 89:20
Mdo 13:22

e 1Sa 16:1
1Fa 1:39

f Hes 11:17
Amu 3:9, 10
1Sa 10:6
2Sa 23:2

g 1Sa 1:1, 19

h 1Sa 18:12
1Sa 28:15

i 1Sa 18:10
1Sa 19:9

j Met 22:29

mbele ya Samweli, lakini Samweli akamwambia Yese: “Yehova hajamchagua yeyote kati ya hawa.”

11 Mwishowe Samweli akamuuliza Yese: “Je, hawa ndio wana wako wote?” Akajibu: “Aliye mdogo zaidi^a ameachwa mpaka sasa; anawalisha kondoo.”^b Kisha Samweli akamwambia Yese: “Mtume mtu akamwite, kwa sababu hatutaketi kula chakula mpaka atakapokuja hapa.” **12** Basi akamtuma mtu amwite, Yese akamleta ndani. Kijana huyo alikuwa mwekundu, mwenye macho yanayovutia, na mwenye sura nzuri.^c Ndipo Yehova akasema: “Simama, mtie mafuta, kwa maana huyu ndiye!”^d

13 Basi Samweli akachukua ile pembe ya mafuta^e na kumtia mafuta mbele ya ndugu zake. Na roho ya Yehova ikaa-nza kumtia nguvu Daudi kuanzia siku hiyo na kuendelea.^f Baadaye Samweli akainuka na kwenda zake Rama.^g

14 Sasa roho ya Yehova ilikuwa imemwacha Sauli,^h na roho mbaya kutoka kwa Yehova ilikuwa ikimtesa.ⁱ **15** Watumishi wa Sauli wakamwambia: “Unaona kwamba roho mbaya kutoka kwa Mungu inakutesa. **16** Tafadhali, bwana wetu, waamuru watumishi wako walio mbele yako wamtafute mtu mwenye ustadi wa kupiga kinubi./ Waka-ti wowote roho mbaya kutoka kwa Mungu inapokujia, atapiga kinubi, nawe utahisi vizuri.” **17** Basi Sauli akawaambia watumishi wake: “Tafadhali, nitafutieni mtu anayepiga kinubi vizuri, mumlete kwangu.”

18 Mtumishi mmoja akasema: "Tazama! Nimeona mwana fulani wa Yese Mbethlehemu anavyopiga kinubi kwa ustadi, ni mtu jasiri na shujaa hodari.^a Ana ustadi wa kuongea, ana sura nzuri,^b na Yehova yuko pamoja naye."^c **19** Ndi-po Sauli akawatuma wajumbe kwa Yese na kumwambia: "Mtume mwana wako Daudi aje kwangu, yule anayechunga kondoo."^d **20** Basi Yese akapakia mikate, kiriba cha ngozi chenye divai, na mwanambuzi juu ya punda, akamtuma Daudi mwana wake kwa Sauli akiwa na vitu hivyo. **21** Kwa hiyo Daudi akafika kwa Sauli na kuanza kumtumikia.^e Sauli akampenda sana, naye Daudi akawa akimbebea silaha zake. **22** Sauli akamtumia Yese ujumbe huu: "Tafadhali, mruhusu Daudi aendeele kunitumikia, kwa sababu amepata kibali machoni pangu." **23** Wakati wowote roho mbaya kutoka kwa Mungu ilipomjia Sauli, Daudi alichukua kinubi na kupiga, kisha Sauli alipata kitulizo na kuhisi vizuri, na roho hiyo mbaya ilimwacha.^f

17 Sasa Wafilisti^g wakakusanya majeshi yao* kwa ajili ya vita. Walikusanyika huko Soko,^h jiji la Yuda, wakapiga kambi kati ya Soko na Azeka,ⁱ kule Efes-damimu.^j **2** Sauli na wanaume wa Israeli wakakusanyika na kupiga kambi katika Bonde la* Ela,^k nao wakajipanga kivita ili kupigana na Wafilisti. **3** Wafilisti walikuwa upande mmoja wa mlima, na Waisraeli walikuwa upande ule mwingi-

17:1 *Tnn., "kambi zao." 17:2 *Tnn., "Nchi Tambarare ya Chini ya."

SURA YA 16

a 1Sa 17:32, 36
1Sa 17:45, 46

b 1Sa 16:12

c 1Sa 18:12

d 1Sa 17:15

e Met 22:29

f 1Sa 16:14
1Sa 18:10
1Sa 19:9

SURA YA 17

g Amu 3:1, 3
1Sa 9:16
1Sa 14:52

h 2Nya 28:18

i Yos 15:20, 35
Yer 34:7

j 1Nya 11:12, 13

k 1Sa 21:9

Safu ya 2

a 1Sa 17:23

b Yos 11:22
2Sa 21:20, 21

c 1Sa 17:38, 39
1Fa 22:34

d 1Sa 17:45

e 1Nya 20:5

f Hes 33:55

g 1Sa 17:26
2Fa 19:22

ne, na bonde lilikuwa katikati yao.

4 Kisha shujaa mmoja akatoka katika kambi za Wafilisti; aliitwa Goliathi,^a kutoka Gathi,^b alikuwa na urefu wa mikonno sita na shubiri moja.* **5** Alikuwa na kofia ya shaba kichwani, naye alivaa koti la vita lenye magamba yanayolaliana. Koti hilo la vita la shaba^c lilikuwa na uzito wa shekeli 5,000.* **6** Alikuwa na mabamba ya shaba yaliyokinga miguu yake na fumo^d la shaba lililoning'inia katikati ya mabega yake. **7** Mpini wa mbao wa mkuki wake ulikuwa kama mti wa wafumaji wa nguo,^e na kichwa cha chuma cha mkuki wake kilikuwa na uzito wa shekeli 600;* na mtu aliye-mbebea ngao alitembea mbele yake. **8** Basi akasimama na kuviita vikosi vya Israeli^f akisema: "Kwa nini mmekuja kujipanga kivita? Je, mimi si Mfilisti nanyi je, si watumishi wa Sauli? Jichagulieni mwanamume, aje kupigana nami. **9** Akiweza kupigana nami na kuniua, tutakuwa watumishi wenu. Lakini nikimshinda na kumuua, mtakuwa watumishi wetu, nanyi mtatutumikia." **10** Kisha Mfilisti huyo akasema: "Ninavitukana* vikosi vya Israeli^g leo. Nipeni mwanamume, nipigane naye!"

11 Sauli na Waisraeli wote waliposikia maneno hayo ya Mfilisti huyo, wakashikwa na hofu na kuogopa sana.

17:4 *Alikuwa na urefu wa mita 2.9 hivi (futi 9 na inchi 5.75). Angalia Nyongeza B14. 17:5 *Karibu kilogramu 57. Angalia Nyongeza B14. 17:7 *Karibu kilogramu 6.84. Angalia Nyongeza B14. 17:10 *Au "Nataka kushindana na."

12 Basi Daudi alikuwa mwana wa Yese,^a Mwefrathi^b kutoka mji wa Bethlehemu^c wa Yuda, ambaye alikuwa na wana wanane^d na ambaye katika siku za Sauli alikuwa tayari amezeeka. 13 Wana watatu wakubwa wa Yese walikuwa wameenda na Sauli vitani.^e Majina ya wana hao watatu walioenda vitani ni Eliabu^f mzaliwa wake wa kwanza, Abinadabu^g mwana wake wa pili, na Shamma mwana wake wa tatu.^h 14 Daudi ndiye aliyekuwa mdogo zaidi,ⁱ na wale watatu wakubwa walikuwa wameenda pamoja na Sauli.

15 Daudi alikuwa akienda na kurudi kutoka kwa Sauli ili kuchunga kondoo^j wa baba yake huko Bethlehemu. 16 Wakati huo, yule Mfilisti alikuwa akija na kuwadhihaki kila asubuhi na kila jioni kwa siku 40.

17 Ndipo Yese akamwambia Daudi mwana wake: "Tafadhali, chukua hii efa* ya nafa-ka iliyokaangwa na mikate hii kumi, uwapelekee haraka ndugu zako kambini. 18 Nawe umpelekee mkuu wa elfu mafungu haya kumi ya jibini;* pia, angalia ndugu zako wanaendeleaje na unilettee kitu fulani kutoka kwao." 19 Walikuwa pamoja na Sauli na wanaume wengine wote wa Israeli katika Bonde la* Ela,^k wakipigana na Wafilisti.^l

20 Kwa hiyo Daudi akaamka asubuhi na mapema na kuwaacha kondoo mikononi mwa mtu mwingine; kisha akapakia vitu hivyo na

17:17 *Efa ilikuwa sawa na lita 22 au kilogramu 13 hivi. Angalia Nyongeza B14. 17:18 *Tnn., "maziwa." 17:19 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

SURA YA 17

a Ru 4:22

b Mwa 35:16, 19
Ru 1:2c 1Sa 17:58
Mik 5:2
Mt 2:6

d 1Nya 2:13-15

e Hes 1:3

f 1Sa 16:6

g 1Sa 16:8

h 1Sa 16:9

i 1Nya 2:13, 15

j 1Sa 16:11, 19

k 1Sa 17:2
1Sa 21:9

l 1Sa 9:16, 17

Safu ya 2

a 1Sa 17:17, 18

b 1Sa 17:4

c 1Sa 17:10

d 1Sa 17:11

e 1Sa 17:10

f Yos 15:16
1Sa 14:49
1Sa 18:17, 21g 1Sa 17:10
Yer 10:10

kwenda kama Yese alivyokuwa amemwamuru. Alipofika kambini, jeshi lilikuwa likiendana kwenye uwanja wa vita huku likipiga kelele za vita. 21 Waisraeli na Wafilisti wakajipanga kivita wakikabiliana uso kwa uso. 22 Mara moja Daudi akaiacha mizigo yake mikononi mwa mtu aliyetunza mizigo, akakimbia kwenda kwenye uwanja wa vita. Alipofika, akaanza kuulizia habari za ndugu zake.^a

23 Alipokuwa akizungumza nao, akaja yule Mfilisti shujaa aliyetwa Goliathi,^b kutoka Gathi. Alitoka katika vikosi vya Wafilisti, akasema maneno yaleyale aliyozoea kusema,^c na Daudi akamsikia. 24 Wanaume wote wa Israeli walipomwona mwanamume huyo, wakaogopa sana na kumkimbia.^d 25 Wanaume wa Israeli walikuwa wakisema: "Je, mnamwona mwanamume yule anayekuja? Anakuja kuwatukana* Waisraeli.^e Mfalme atampa utajiri mwingi mtu atakayemuua mwanamume huyo, atampa pia binti yake mwenyewe,^f naye ataiondolea wajibu nyumba ya baba yake katika Israeli."

26 Daudi akaanza kuwauliza wanaume waliokuwa wamesimama karibu naye: "Mtu atakayemuua yule Mfilisti na kuwaondolea Waisraeli aibu atafanyiwa nini? Kwani huyu Mfilisti asiyetahiriwa ni nani hata avitukane* vikosi vya Mungu aliye hai?"^g 27 Basi watu hao wakamwambia maneno yaleyale yaliyokuwa yamesemwa: "Hivi ndivyo

17:25 *Au "kushindana na." 17:26 *Au "ashindane na."

atakavyofanyiwa mwanamume atakayemua.” **28** Eliabu ndugu yake mkubwa^a alipomsikia Daudi akizungumza na wanaume hao, akamkasirikia Daudi na kumwambia: “Kwa nini umeshuka huku? Na wale kondoo wachache nyikani umemwachia nani?^b Najua vizuri kimbelebele chako na nia mbaya ya moyo wako; umeshuka tu ili kutazama vita.” **29** Daudi akamwambia: “Sasa nimefanya nini? Nilikuwa nikiuliza swali tu!” **30** Ndipo Daudi akamwacha, akamgeukia mtu mwingine na kumuuliza swali lilelile,^c na watu wakamjibu vilevile kama mwanzoni.^d

31 Watu wakasikia maneno aliyosema Daudi, wakamwambia Sauli. Basi Sauli akaagiza aitwe. **32** Daudi akamwambia Sauli: “Mtu yeyote asife moyo* kwa sababu yake. Mimi mtumishi wako nitaenda kupigana na huyo Mfilisti.”^e **33** Lakini Sauli akamwambia Daudi: “Huwezi kwenda kupigana na huyo Mfilisti, kwa sababu wewe ni mvulana tu,^f naye amekuwa mwanajeshi* tangu alipokuwa kijana.” **34** Ndipo Daudi akamwambia Sauli: “Mimi mtumishi wako nimekuwa nikichunga kondoo wa baba yangu, na simba^g akaja, na pia dubu, na kila mmoja wao akamchukua kondoo kutoka kundini. **35** Nilimfuata, nikamua na kumwokoia kondoo kutoka kinywani mwake. Aliporuka ili kunishambulia, nilimkamata manyoya yake,* nikampiga, na kumua. **36** Mimi mtumishi

17:32 *Au “asiogope.” 17:33 *Au “mwanamume wa vita.” 17:35 *Au “utaya wake.” Tnn., “ndeve zake.”

SURA YA 17

a 1Sa 16:6, 7
1Nya 2:13

b 1Sa 17:20

c 1Sa 17:26

d 1Sa 17:25

e 1Sa 16:18

f 1Sa 17:42

g Isa 31:4

Safu ya 2

a 1Sa 17:10
Yer 10:10

b Kum 7:21
2Fa 6:16
Ebr 11:32-34

c Amu 20:15, 16

d 1Sa 16:12
1Sa 17:33

e 1Sa 24:14
2Sa 16:9
2Fa 8:13

wako nilimua simba na dubu pia, na huyu Mfilisti asiyetahiririwa atakuwa kama mmoja wao, kwa sababu amevitukana* vikosi vya Mungu aliye hai.”^a **37** Kisha Daudi akasema: “Yehova, aliyeniokoa kutoka katika makucha ya simba na ya dubu, ndiye atakayeniokoa kutoka mikononi mwa Mfilisti huyo.”^b Ndipo Sauli akamwambia Daudi: “Nenda, na Yehova awe pamoja nawe.”

38 Basi Sauli akamvisha Daudi mavazi yake. Akamvisha kofia ya shaba kichwani, halafu akamvisha koti la vita. **39** Kisha Daudi akajifunga upanga wake juu ya mavazi yake, akajaribu kutembea lakini akashindwa kwa sababu hakuwa ameyazoea. Basi Daudi akamwambia Sauli: “Siwezi kwenda nikiwa nimevaa vitu hivi, kwa maana sijavizoea.” Kwa hiyo Daudi akavivua. **40** Kisha akachukua fimbo yake mkononi, akajichagulia mawe matano laini kutoka katika bonde la kijito, akayaweka kwenye kifuko ndani ya mfuko wake wa mchungaji, na kombeo^c lili kuwa mkononi mwake. Naye akaanza kumkaribia huyo Mfilisti.

41 Mfilisti huyo akaanza kumkaribia Daudi zaidi na zaidi, na mtu aliyembebea ngao alikuwa mbele yake. **42** Mfilisti huyo alipotazama na kumwona Daudi, akaanza kumdhihakiki kwa dharau kwa sababu alikuwa tu mvulana mwekundu mwenye sura nzuri.^d **43** Basi Mfilisti huyo akamuuliza Daudi: “Je, mimi ni mbwa^e hivi kwamba unijie

17:36 *Au “ameshindana na.”

na vijiti?" Ndipo huyo Mfilisti akamlaani Daudi kwa miungu yake. **44** Akamwambia Daudi: "Nikaribie tu, nyama yako nitawapa ndege wa angani na wanyama wa mwituni."

45 Daudi akamjibu hivi huyo Mfilisti: "Unakuja kupigana nami kwa upanga, mkuiki, na fumo,^a lakini mimi naja kupigana nawe kwa jina la Yehova wa majeshi,^b Mungu wa vikosi vya Israeli, ambaye umemtukana."^c **46** Siku hii ya leo Yehova atakutia wewe mikononi mwangu,^d nami nitakuu na kukata kichwa chako; na siku ya leo nitawapa ndege wa angani na wanyama mwiu wa dunia maiti za kambi ya Wafilisti; na watu wote duniani watajua kwamba kuna Mungu katika Israeli.^e **47** Na watu wote waliokusanyika hapa watajua* kwamba Yehova haokoi kwa upanga wala kwa mkuki,^f kwa sababu vita ni vya Yehova,^g naye atawatia ninyi nyote mikononi mwetu."^h

48 Basi Mfilisti huyo akasimama, akazidi kukaribia ili akutane na Daudi, lakini Daudi akakimbia haraka kuelekea kwenye uwanja wa vita kukutana na Mfilisti huyo. **49** Daudi akautia mkono wake ndani ya mfuko wake, akachukua jiwe kutoka humo, na kulirusha kwa kombeo. Akampiga Mfilisti huyo kwenye paji la uso, na jiwe hilo likapenya katika paji la uso wake, akaanguka chini kifufufudi.ⁱ **50** Basi Daudi akamshinda Mfilisti huyo kwa kombeo na jiwe; alimpiga Mfilisti

17:45 *Au "umeshindana naye." 17:47 *Tnn., "Na kutaniko hili lote litajua."

SURA YA 17

a 1Sa 17:4, 6

b 2Sa 5:10
Ebr 11:32-34c 1Sa 17:10
2Fa 19:22d Kum 9:1-3
Yos 10:8e Kut 9:16
Kum 28:10
1Fa 8:43
2Fa 19:19
Da 3:29f Zb 44:6, 7
Zek 4:6g 2Nya 20:15
Met 21:31

h Kum 20:4

i 1Sa 17:37
2Sa 21:22

Safu ya 2

a Amu 3:31
Amu 15:15, 16
1Sa 17:47

b 1Sa 21:9

c Kum 28:7
Yos 23:10
Ebr 11:32-34

d 1Sa 17:2, 19

e Yos 15:20, 45

f Yos 15:20, 36

g 1Sa 21:9

h 1Sa 14:50

i 1Sa 16:19, 21

j 1Sa 17:54

huyo na kumuua, ingawa Daudi hakuwa na upanga mkononi mwake.^a **51** Daudi akaendelea kukimbia na kusimama juu yake. Kisha akaushika upanga wa Mfilisti^b huyo na kucho-moa kutoka katika ala yake, akahakikisha kwamba amekufa kwa kumkata kichwa kwa upanga huo. Wafilisti walipoo-na kwamba shujaa wao amekufa, wakakimbia.^c

52 Kisha wanaume wa Israeli na Yuda wakainuka na kuanza kupiga kelele na kuwafuatia Wafilisti kuanzia bondeni^d mpaka kwenye malango ya Ekroni,^e na maiti za Wafilisti waliouawa zilienea barabara-ni kuanzia Shaaraimu,^f mpaka Gathi na Ekroni. **53** Waisraeli waliporudi baada ya kuwafuatia vikali Wafilisti, walipora kambi zao.

54 Halafu Daudi akachukua kichwa cha yule Mfilisti na kukileta Yerusalemu, lakini akaziweka silaha za Mfilisti huyo ndani ya hema lake mwenyewe.^g

55 Sauli alipomwona Daudi akienda kupigana na Mfilisti huyo, alimuuliza hivi Abneri^h mkuu wa jeshi: "Abneri, mvulana huyu ni mwana wa nani?" Abneri akajibu: "Kwa hakika kama unavyoishi,* Ee mfalme, mimi sijui!"

56 Mfalme akasema: "Tafuta mvulana huyu ni mwana wa nani." **57** Basi mara tu Daudi aliporudi baada ya kumuua huyo Mfilisti, Abneri akamchukua na kumpeleka mbele ya Sauli akiwa na kichwa cha huyo Mfilistiⁱ mkononi mwake. **58** Ndipo Sauli akamuuliza: "Mvulana, wewe ni mwa-

17:55 *Au "Kama nafsi yako inavyoishi."

na wa nani?" Daudi akamjibu: "Mimi ni mwana wa mtumishi wako Yese^a Mbethlehemu."^b

18 Baada tu ya Daudi kumaliza kuzungumza na Sauli, Yonathani^c na Daudi wakashikamana na kuwa marafiki wa karibu sana,^{*} na Yonathani akaanza kumpenda kama alivyojipenda mwenyewe.^{#d} **2** Kuanzia siku hiyo, Sauli akamchukua Daudi, naye hakumruhusu arudi nyumbani kwa baba yake.^e **3** Na Yonathani na Daudi wakafanya agano,^f kwa sababu alimpenda kama alivyojipenda mwenyewe.^{#g} **4** Yonathani akavua joho lake lililo na mikono na kumpa Daudi, pamoja na silaha zake, upanga wake, upinde wake, na mshipi wake. **5** Daudi akaanza kwenda vitani, naye alifanikiwa^{*h} popote alipotumwa na Sauli. Basi Sauli akamweka asimamie wanajeshi vitani,ⁱ na jambo hilo likawafurahisha watu wote na pia watumishi wa Sauli.

6 Daudi na watu wengine walipokuwa wakirudi baada ya kuwaua Wafilisti, wanawake walikuwa wakitoka kati majiji yote ya Israeli wakimba^j na kucheza dansi ili kumpokea Mfalme Sauli kwa matari,^k kwa vigelegele, na udi. **7** Wanawake hao waliokuwa wakisherehekea walikuwa wakimba hivi:

"Sauli ameuwa maelfu yake,
Na Daudi makumi yake ya
maelfu."^l

8 Sauli akakasirika sana,^m na wimbo huo haukumpendeza

18:1 *Au "nafsi ya Yonathani ikashikamana na nafsi ya Daudi." **18:1, 3** #Au "kama nafsi yake mwenyewe." **18:5** *Au "alitenda kwa hekima."

SURA YA 17

a Ru 4:22
1Sa 16:1
1Nya 2:13, 15
Mt 1:6
Lu 3:23, 32
Mdo 13:22

b 1Sa 17:12

SURA YA 18

c 1Sa 14:1, 49

d 1Sa 19:2
1Sa 20:17, 41
2Sa 1:26

e 1Sa 8:11
1Sa 16:22
1Sa 17:15

f 1Sa 20:8, 42
1Sa 23:18
2Sa 9:1
2Sa 21:7

g Met 17:17
Met 18:24

h 1Sa 18:30

i 1Sa 14:52

j Kut 15:20, 21
Amu 5:1

k Amu 11:34

l 1Sa 21:11
1Sa 29:5

m Mwa 4:5
Met 14:30

Safu ya 2

a 1Sa 13:14
1Sa 15:27, 28
1Sa 16:13
1Sa 20:31
1Sa 24:17, 20

b 1Sa 16:14

c 1Sa 16:16, 23

d 1Sa 19:9, 10

e 1Sa 20:33

f 1Sa 18:28, 29

g 1Sa 16:14

h 2Sa 5:2

i 1Sa 18:5

j Mwa 39:2
Yos 6:27
1Sa 10:7
1Sa 16:18

k 1Sa 14:49

l 1Sa 17:25

m 1Sa 25:28

kwa kuwa alisema: "Wame-mpa Daudi makumi ya maelfu, lakini mimi wamenipa maelfu. Lililobaki tu ni kumpa ufalme!"^a **9** Kuanzia siku hiyo na kuendelea, Sauli alikuwa aki mtilia shaka Daudi.

10 Siku iliyofuata, roho mbaya kutoka kwa Mungu ikamvamia Sauli,^b naye akaanza kutenda kwa njia ya ajabu^{*} nyumbani, huku Daudi akipiga muziki kwa kinubi^c kama alivyofanya nyakati nyingine. Sauli alikuwa na mkuki mkononi,^d **11** basi akaurusha mkuki huo^e akisema hivi moyoni: 'Nitampigilia Daudi ukutani!' Lakini Daudi alimkwepa mara mbili. **12** Ndi-po Sauli akamwogopa Daudi kwa sababu Yehova alikuwa pamoja naye^f lakini alikuwa amemwacha yeye.^{*g} **13** Kwa hiyo Sauli akamwondoa nyumbani mwake na kumweka kuwa mkuu wa elfu, basi Daudi alikuwa akiliongoza jeshi vitani.^{*h} **14** Daudi akaendelea kufanikiwa^{*i} kati-ka mambo yote aliyofanya, na Yehova alikuwa pamoja naye.^j **15** Sauli alipoona kwamba Daudi anafanikiwa sana, akaanza kumwogopa. **16** Lakini watu wote wa Israeli na Yuda walimpenda Daudi, kwa sababu alikuwa akiwaongoza vitani.

17 Baadaye Sauli akamwambia Daudi: "Ndiye huyu Merab binti yangu mkubwa,^k Nitakupa awe mke wako.^l Lakini unapaswa kuendelea kunitumikia kwa ujasiri na kupigana vita vya Yehova."^m Kwa maana

18:10 *Au "kutenda kama nabii." **18:12** *Yaani, Sauli. **18:13** *Tnn., "akitoka nje na kuingia mbele ya watu." **18:14** *Au "kutenda kwa hekima."

Sauli alisema hivi moyoni: 'Mkono wangu usimuu. Acha mikono ya Wafilisti imuue.'^a

18 Ndipo Daudi akamwambia Sauli: "Mimi ni nani na watu wangu wa ukoo ni nani, au familia ya baba yangu katika Israeli, hata mfalme awe baba mkwe wangu?"^b **19** Hata hivyo, wakati ulipofika wa kumpa Daudi Merabu, binti ya Sauli, tayari Adrieli^c Mmeholathi alikuwa amepewa binti huyo awe mke wake.

20 Sasa Mikali^d binti ya Sauli alimpenda Daudi, Sauli akajulishwa jambo hilo, nalo likampendeza. **21** Kwa hiyo Sauli akasema: "Nitampa Daudi binti huyo ili awe mtego kwake, na ili mikono ya Wafilisti imuue."^e Kisha Sauli akamwambia hivi Daudi mara ya pili: "Utafanya mapatano ya ndoa pamoja nami* leo." **22** Pia, Sauli akawaamuru hivi watumishi wake: "Zungumzeni na Daudi kwa siri na kumwambia, 'Tazama! Mfalme anakupenda, na watumishi wake wote wanakupenda sana. Basi sasa fanya mapatano ya ndoa na mfalme.'" **23** Watumishi wa Sauli walipomwambia Daudi mambo hayo, Daudi akasema: "Je, mnafikiri ni jambo rahisi kwa mtu maskini na asiyeheshimiwa sana kama mimi kufanya mapatano ya ndoa na mfalme?"^f **24** Kisha watumishi wa Sauli wakamletea habari hii: "Haya ndiyo maneno aliyosema Daudi."

25 Kwa hiyo Sauli akasema: "Hivi ndivyo mnavyopaswa kumwambia Daudi: 'Mfalme hataki mahari yoyote^g isipoku-

18:21 *Au "Nitakuwa baba mkwe wako."

SURA YA 18

a 1Sa 18:25

b 2Sa 7:18

c 2Sa 21:8

d 1Sa 14:49
1Sa 19:11
1Sa 25:44
2Sa 3:13
2Sa 6:16

e 1Sa 18:17

f 1Sa 18:18

g Mwa 29:18

Safu ya 2

a 1Sa 17:26, 36
2Sa 3:14

b 1Sa 18:21

c 1Sa 17:25

d 1Sa 16:13
1Sa 24:17, 20

e 1Sa 18:20

f 1Sa 18:9, 12
1Sa 20:33

g 1Sa 18:5

h 2Sa 7:9

SURA YA 19

i 1Sa 18:9
Met 27:4j 1Sa 18:1
Met 18:24

wa magovi 100 ya Wafilisti,^a ili mfalme awalipize kisasi madaui wake." Lakini Sauli alikuwa anapanga njama ili Wafilisti wamuue Daudi. **26** Basi watumishi wake wakamwambia Daudi habari hiyo, na habari hiyo ya kufanya mapatano ya ndoa na mfalme ikampendeza Daudi.^b Kabla ya siku ili yopangwa kufika, **27** Daudi alienda na wanaume wake na kuwaua wanaume 200 Wafilisti, na Daudi akamletea mfalme idadi kamili ya magovi yao, ili afanye mapatano ya ndoa na mfalme. Basi Sauli akampa Daudi Mikali binti yake awe mke wake.^c **28** Sauli akatambua kwamba Yehova alikuwa pamoja na Daudi^d na Mikali binti yake alimpenda Daudi.^e **29** Jambo hilo likamfanya Sauli azidi kumwogopa Daudi, basi Sauli akawa adui ya Daudi maisha yake yote.^f

30 Watawala wa Wafilisti walikuwa wakienda vitani, lakini kadiri walivyoenda, ndivyo Daudi alivyozidi kufanikiwa* kuliko watumishi wote wa Sauli;^g na jina lake liliheshimiwa sana.^h

19 Baadaye Sauli akazungumza na Yonathani mwana wake na watumishi wake wote kuhusu kumuua Daudi.ⁱ **2** Kwa kuwa Yonathani mwana wa Sauli alimpenda sana Daudi,^j alimwambia hivi Daudi: "Sauli baba yangu anakusudia kukuua. Tafadhali jihadhari itakapofika asubuhi, nenda mahali pa siri na ujifiche huko. **3** Nitakuja na kusimama kando ya baba yangu shambani mahali utaka-

18:30 *Au "alivyozidi kutenda kwa hekima."

pokuwa. Nitaongea na baba yangu kukuhusu, nikipata habari yoyote, bila shaka nita kuambia.”^a

4 Basi Yonathani akamsifu Daudi^b mbele ya Sauli baba yake. Akamwambia: “Mfalme, usimtendee dhambi mtumishi wako Daudi kwa sababu yeye hajakutendea dhambi na mambo aliyokufanyia yamekunufaisha. **5** Alihatarisha uhai wake* alipomuua yule Mfilisti,^c na Yehova akawapa Waisraeli wote ushindi[#] mku-bwa. Ulionga jambo hilo, ukashangilia sana. Basi kwa nini uitendee dhambi damu isiyo na hatia kwa kuagiza Daudi auawe bila sababu?”^d **6** Sauli akamsikiliza Yonathani na kuapa hivi: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, hatauawa.” **7** Baadaye Yonathani akamwita Daudi na kumwambia mambo hayo yote. Kisha Yonathani akampeleka Daudi kwa Sauli, naye akaendelea kumtumikia kama awali.^e

8 Baada ya muda vita vika-tokea tena, na Daudi akaenda kupigana na Wafilisti na kuwaua Wafilisti wengi sana, nao wakakimbia kutoka mbele yake.

9 Na roho mbaya kutoka kwa Yehova ikamjia Sauli^f alipokuwa ameketi nyumbani mwake akiwa na mkuki mkononi, huku Daudi akipiga muziki kwa kinubi.^g **10** Sauli akajaribu kumpigilia Daudi ukutani kwa mkuki, lakini akamkwepa Sauli, na mkuki huo ukapenya ukutani. Daudi akakimbia na kutoroka usiku huo. **11** Baadaye Sauli aka-

19:5 *Au “Aliitia nafsi yake mikononi mwake.” [#]Au “wokovu.”

SURA YA 19

a 1Sa 20:9,13
Met 17:17

b 1Sa 22:14

c 1Sa 17:49

d 1Sa 20:32

e 1Sa 16:21
1Sa 18:2,13

f 1Sa 16:14

g 1Sa 18:10,11

Safu ya 2

a Zb 59:Uta, 3

b 1Sa 18:9

c 1Sa 18:29

d 1Sa 7:15,17

e 1Sa 20:1

watuma wajumbe nyumbani kwa Daudi ili wailinde na kumuua asubuhi,^a lakini Mikali mke wa Daudi akamwambia Daudi: “Usipotoroka usiku wa leo, kesho utakuwa mfu.” **12** Mara moja Mikali akamtemremsha Daudi kupitia dirishani, ili akimbie na kutoroka. **13** Mikali akachukua sanamu ya terafimu* na kuiweka kitandani, akaifunika kwa vazi na kuweka wavu wa manyoya ya mbuzi mahali ambapo Daudi hulaza kichwa chake.

14 Basi Sauli akawatuma wajumbe wamlete Daudi, lakini mke wa Daudi akawaambia: “Ni mgonjwa.” **15** Kisha Sauli akawatuma wajumbe hao wamwone Daudi, akawaambia: “Mleteni kwangu akiwa kwenye kitanda chake ili auawe.”^b **16** Wajumbe hao walipoingia, walikuta sanamu ya terafimu* kitandani na wavu wa manyoya ya mbuzi mahali anapolaza kichwa chake. **17** Sauli akamuliza Mikali: “Kwa nini ulinidanganya hivi na kumwacha adui yangu^c akimbie na kutoroka?” Mikali akamjibu Sauli: “Aliniambia, ‘Niache niende, nisije nikakuu!’”

18 Basi Daudi alikimbia na kutoroka, akafika kwa Samweli kule Rama.^d Akamwambia mambo yote ambayo Sauli alikuwa amemtendea. Kisha yeye na Samweli wakaeenda zao, wakakaa kule Naiothi.^e **19** Baada ya muda Sauli aliambiwa hivi: “Tazama! Daudi yuko Naiothi kule Rama.” **20** Mara moja Sauli akawatuma wajumbe wamkamate Daudi. Walipowaona manabii waliozeeka wakitoa

19:13, 16 *Au “mungu wa familia; sanamu.”

unabii na Samweli akiwa amesimama na kuwaongoza, roho ya Mungu ikawajia wajumbe wa Sauli, nao pia wakaanza kutenda kama manabii.

21 Walipomwambia Sauli habari hizo, mara moja akawatumama wajumbe wengine, nao pia wakaanza kutenda kama manabii. Basi Sauli akawatumama tena wajumbe wengine, kikundi cha tatu, nao pia wakaanza kutenda kama manabii. **22** Mwishowe yeye pia akaenda Rama. Alipofika kwenye tangi kubwa la maji lililoko Seku, akauliza: “Samweli na Daudi wako wapi?” Wakamjibu: “Wako Naiothi^a kule Rama.” **23** Sauli alipokuwa njiani kutoka huko kwenenda Naiothi kule Rama, roho ya Mungu ikamjia pia, naye akatembea huku akitenda kama nabii mpaka alipoingia Naiothi kule Rama. **24** Akararua pia mavazi yake, naye pia akatenda kama nabii mbele ya Samweli, akalala huko mchana wote na usiku huo wote akiwa uchi.* Ndiyo sababu wanasema: “Je, Sauli pia ni mmoja wa manabii?”^b

20 Kisha Daudi akakimbia kutoka Naiothi huko Rama. Hata hivyo, akaenda kwa Yonathani na kumuuliza: “Nimefanya nini?”^c Nimefanya kosa gani, nami nime mtendea baba yako dhambi gani hivi kwamba anataka kuniua?” **2** Yonathani akamwambia: “Ni jambo lisiloweza kuwaziwa kamwe!^d Huta kufa. Baba yangu hawezi kufanya jambo lolote, liwe kubwa au dogo, bila kuniambia. Kwa nini baba yangu anifi-

SURA YA 19

a 1Sa 19:18

b 1Sa 10:11

SURA YA 20

c 1Sa 24:11
Zb 18:20

d 1Sa 19:6

Safu ya 2

a 1Sa 18:1
1Sa 19:2

b 1Sa 27:1

c Hes 10:10
2Nya 2:4

d 1Sa 16:4, 18

e 1Sa 20:28, 29

f Met 17:17

g 1Sa 18:3
1Sa 23:18

h 1Sa 20:1

i 1Sa 19:2

che jambo hilo? Hawezi kufanya hivyo.” **3** Lakini Daudi akaapa hivi tena: “Bila shaka baba yako anajua kwamba unanipenda^a na hivyo atasema, ‘Msimwambie Yonathani jambo hili asije akahuzunika.’ Lakini kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kwa hakika kama unavyoishi,* kuna hatua moja tu kati yangu na kifol!”^b

4 Ndipo Yonathani akamwambia Daudi: “Nitakufanyia lolote unalosema.” **5** Daudi akamwambia Yonathani: “Kesho ni mwezi mpya,^c na hakika ninatazamiwa kuketi pamoja na mfalme ili kula naye; niache niende, nitajificha shambani mpaka siku ya tatu jioni. **6** Ikiwa baba yako atanikosa, mwambie, ‘Daudi alinisihi nimruhusu aende mara moja katika jiji lake la Bethlehemu,^d kwa sababu kuna dhabihu ya kila mwaka huko kwa ajili ya familia yote.’^e **7** Aki sema, ‘Ni vema!’ mimi mtumishi wako nitakuwa na amani. Lakini akikasirika, uwe na hakika kwamba amezimia kunidhuru. **8** Nitendee mimi mtumishi wako kwa upe ndo mshikamanifu,^f kwa kuwa umeniingiza mimi mtumishi wako katika agano ulilofanya na Yehova.^g Lakini ikiwa nina hatia,^h niue wewe mwenyewe. Kwa nini unitie mikononi mwa baba yako?”

9 Kwa hiyo Yonathani akasema: “Ni jambo nisiloweza kamwe kuwazia kwamba nipendekeze utendewe hivyo! Nikipata habari kwamba baba yangu amezimia kukudhuru, kwa nini nisikwambie?”ⁱ **10** Kisha Daudi aka-

19:24 *Au “akiwa na mavazi machache.”

20:3 *Au “nafsi yako inavyoishi.”

muuliza Yonathani: “Ni nani atakayeniambia baba yako akikujibu kwa ukali?” **11** Yonathani akamwambia Daudi: “Njoo, twende shambani.” Basi wote wawili wakaenda shambani. **12** Yonathani akamwambia Daudi: “Yehova Mungu wa Israeli na awe shahidi kwamba nitamchunguza baba yangu wakati kama huu kesho au siku ya tatu. Ikiwa ana mtazamo mzuri kukuelekea, je, sitakujulisha au kukufunulia jambo hilo?” **13** Lakini ikiwa baba yangu anakusudia kukudhuru, Yehova na ania-dhibu, tena vikali, ikiwa sitakufunulia jambo hilo na kucha uende zako kwa amani. Yehova na awe pamoja nawe,^a kama alivyokuwa na baba yangu.^b **14** Na je, hutanite-ndea kwa upendo mshikamanifu wa Yehova ningali hai na hata nikifa?^c **15** Usiache kamwe kuitendea nyumba yangu kwa upendo mshikamanifu,^d hata Yehova atakapowafagilia mbali maadui wote wa Daudi duniani pote.” **16** Basi Yonathani akafanya agano pamoja na nyumba ya Daudi, akisema: “Yehova atadai jambo hilo na kuwaadhibu maadui wa Daudi.” **17** Basi Yonathani akamwapisha tena Daudi kwa msingi wa upendo alikuwa nao kumwelekea, kwa sababu alimpenda kama alivyojipenda mwenyewe.*^e

18 Kisha Yonathani akamwambia: “Kesho ni mwezi mpya,^f nawe utakosekana kwa sababu kiti chako kitakuwa wazi. **19** Kufikia siku ya tatu, wataona wazi kwamba hau-po, utakuja mahali hapa uli-

20:17 *Au “kama nafsi yake mwenyewe.”

SURA YA 20

a 1Sa 16:13
1Sa 17:37

b 1Sa 10:7
1Sa 11:6

c 2Sa 9:1, 3
2Sa 9:6, 7

d 2Sa 21:7

e 1Sa 18:1, 3
2Sa 1:26
Met 18:24

f 1Sa 20:5

Safu ya 2

a 1Sa 20:13, 14

b 1Sa 20:42

c 1Sa 20:5

d 1Sa 14:50

e Law 11:23, 24
Law 15:4, 5
Law 15:16, 18
Hes 19:16

f 1Sa 17:12

pojificha ile siku nyingine* na ukae hapa karibu na jiwe. **20** Kisha nitapiga mishale mitatu upande mmoja wa jiwe hili kana kwamba ninale-nga shabaha fulani. **21** Nita-kapomtuma mtumishi, nitase-ma, ‘Nenda, ukaitafute mishale.’ Nikimwambia mtumishi, ‘Angalia! Mishale iko upande huu wako, ichukue,’ basi una-weza kurudi, kwa maana kwa hakika kama Yehova anavyoi-shi, hilo linamaanisha kwamba kuna amani katika mambo yako yote na hakuna hatari. **22** Lakini nikimwambia mvulana huyo, ‘Angalia! Mishale iko mbele yako,’ basi ondoka, kwa sababu Yehova anataka uende zako. **23** Kuhusu ahadi ambayo tumeweka,^a mimi na wewe, Yehova na awe kati yetu milele.”^b

24 Basi Daudi akajificha shambani. Mwezi mpya ulipofika, mfalme aliketi kwenye kiti chake ili ale.^c **25** Mfalme alikuwa ameketi mahali pake alipoketi kwa kawaida karibu na ukuta. Yonathani aliketi kumwelekea, na Abneri^d aliketi kando ya Sauli, lakini mahali pa Daudi palikuwa wazi. **26** Sauli hakusema lolote siku hiyo, kwa maana alisema moyoni mwake: ‘Jambo fulani limetokea ambalo limemfanya asiwe safi.^e Naam, yeye si safi.’ **27** Siku ya pili baada ya mwezi mpya, bado mahali pa Daudi palikuwa wazi. Kwa hiyo Sauli akamuuliza Yonathani mwana wake: “Kwa nini mwana wa Yese^f hakuja kwenye mlo jana wala leo?” **28** Yonathani akamjibu Sauli: “Daudi alinisihi nimruhusu

20:19 *Tnn., “siku ya kazi.”

aende Bethlehemu.^a **29** Ali-niambia, ‘Tafadhali niruhusu niende, kwa sababu tuna dhabihu ya familia jijini, na ndugu yangu mwenyewe ali-niita. Basi ikiwa nimepata ki-bali machoni pako, tafadhali acha niende kisiri nikawaone ndugu zangu.’ Ndiyo sababu hajaja kwenye meza ya mfal-me.” **30** Kisha Sauli akamka-sirikia Yonathani na kumwamb-ia: “Wewe mwana wa mwanamke mwasi, unafikiri sijui kwamba umeamua kumuunga mkono mwana wa Yese, kwa aibu yako mwenyewe na kwa aibu ya mama yako?” **31** Maadamu mwana wa Yese anaishi duniani, wewe wala ufalme wako hautadumu.^b Basi sasa mtume mtu fulani amlete kwangu, kwa maana lazima afe.”^c

32 Hata hivyo, Yonathani akamwambia Sauli baba yake: “Kwa nini auawe?”^d Amefanya nini?” **33** Ndipo Sauli akamtupia mkuki ili amue,^e basi Yonathani akajua kwamba baba yake alikuwa ameamua kumuua Daudi.^f **34** Yonathani akainuka mara moja kuto-ka mezani akiwa amekasirika sana, naye hakula chakula chochote siku ya pili baada ya mwezi mpya, kwa maana alikuwa amehuzunika sana kwa sababu ya Daudi^g na kwa sababu baba yake mwenyewe alikuwa amemwaibisha.

35 Asubuhi Yonathani akae-nda shambani kukutana na Daudi kama walivyokubaliana, na mtumishi fulani kijana alikuwa pamoja naye.^h **36** Akamwambia mtumishi wake: “Ta-

20:30 *Tnn., “kwa aibu ya uchi wa mama yako?” 20:31 *Tnn., “kwa maana yeye ni mwana wa kifo.”

SURA YA 20

a 1Sa 20:6

b 1Sa 18:8

c 1Sa 19:6, 10

d 1Sa 19:5
Met 17:17
Met 18:24e 1Sa 18:11
1Sa 19:10

f 1Sa 20:6, 7

g 1Sa 18:1

h 1Sa 20:19-22

Safu ya 2

a 1Sa 20:17, 23

b 1Sa 23:18
2Sa 9:7

SURA YA 21

c 1Sa 22:9, 19

fadhali kimbia utafute mishale nitakayopiga.” Mtumishi huyo akakimbia, kisha Yonathani akapiga mshale mbele yake. **37** Mtumishi huyo alipofika mahali ambapo Yonathani alikuwa amepiga mshale, Yonathani akamwambia hivi mtumishi huyo kwa sauti: “Mshale uko mbele yako!” **38** Yonathani akaendelea kumwambia mtumishi huyo kwa sauti: “Fanya haraka! Kimbia! Usikawie!” Mtumishi wa Yonathani akaikota ile mishale na kurudi kwa bwana wake. **39** Lakini mtumishi huyo hakuelewa lolote kuhusu jambo hilo; Yonathani na Daudi peke yao ndio walioelewa jambo hilo. **40** Kisha Yonathani akampa mtumishi wake silaha zake na kumwambia: “Nenda, zipeleke jijini.”

41 Mtumishi huyo alipoo-ndoka, Daudi akatoka mahali alipokuwa amejificha hapo karibu upande wa kusini. Kisha akaanguka chini kifudufudi na kuinama mara tatu, nao wakabusiana na kulia pamoja, lakini Daudi alilia zaidi. **42** Yonathani akamwambia Daudi: “Nenda kwa amani, kwa maana sote wawili tumeapa^a kwa jina la Yehova tukisema, ‘Yehova na awe kati yangu na wewe na kati ya uzao wangu’ na uzao wako[#] milele.”^b

Kisha Daudi akainuka na kuondoka, naye Yonathani akarudi jijini.

21 Baadaye Daudi akafika Nobu^c kwa kuhani Ahimeleki. Ahimeleki alianza kutetemeka alipokutana na Dau-

20:42 *Tnn., “mbegu yangu.” #Tnn., “mbegu yako.”

di, akamuuliza: “Kwa nini uko peke yako na hujaja na mtu yeyote?”^a **2** Daudi akamjibu kuhani Ahimeleki: “Mfalme aliniagiza nifanye jambo fulani, lakini akaniambia, ‘Usimjulishe mtu yeyote kazi niliyokutuma kufanya na maagizo niliyokupa.’ Nilikubaliana na vijana wangu tukutane mahali fulani. **3** Sasa ikiwa una mikate mitano, nipe tu, au chochote kinachopatikana.” **4** Lakini kuhani akamwambia Daudi: “Kwa sasa hakuna mikate ya kawaida, lakini kuna mikate mitakatifu^b—ninaweza kukupa tu ikiwa vijana wako wamejipusha na wanawake.”^{*c} **5** Daudi akamwambia hivi kuhani: “Kwa hakika tumejitenga kabisa na wanawake kama tulivyofanya awali nilipoenda vitani.^d Ikiwa miili ya vijana hawa ni mitakatifu hata katika shughuli za kawaida, je, si mitakatifu zaidi leo?” **6** Basi kuhani akampa mikate mitakatifu,^e kwa sababu hakukuwa na mikate mingine isipokuwa mikate ya woyesho iliyokuwa imeondolewa mbele za Yehova na mikate mipya kuwekwa siku hiyo.

7 Basi mmoja wa watumishi wa Sauli alikuwa hapo siku hiyo, akiwa amezuiliwa mbele za Yehova. Aliitwa Doeg^f Mwedomu,^g mkuu wa wachungaji wa Sauli.

8 Basi Daudi akamuuliza Ahimeleki: “Je, una mkuki au upanga hapa? Sikubeba upanga wangu wala silaha zangu kwa sababu kazi ya mfalme ilipaswa kufanywa haraka.” **9** Ndipo kuhani akamwambia: “Nina upanga wa Goliathi^h

21:4 *Au “hawajafanya ngono.”

SURA YA 21

a 1Sa 18:13

b Kut 25:30
Law 24:5, 9
Mt 12:3, 4c Kut 19:15
Law 15:16
2Sa 11:11

d Law 15:18

e Law 24:7-9
Mk 2:25, 26
Lu 6:3, 4f 1Sa 22:9
Zb 52:Uta

g Mwa 36:1

h 1Sa 17:51, 54

Safu ya 2

a 1Sa 17:2, 50

b Kut 28:6

c 1Sa 27:1

d Yos 11:22
1Sa 5:8
1Sa 17:4
1Sa 27:2
Zb 56:Utae 1Sa 18:6-8
1Sa 29:4, 5

f Zb 56:3, 6

g Zb 34:Uta

SURA YA 22

h 1Sa 21:10

i Yos 15:20, 35
2Sa 23:13
Zb 34:19
Zb 56:13

yule Mfilisti, uliyemuaa katika Bonde la* Ela,^a nao umefungwa kwa kitambaa nyuma ya efodi.^b Ikiwa unataka kuu-chukua, uchukue, kwa sababu ndio upanga pekee ulio hapa.” Daudi akamwambia: “Hakuna upanga mwingine kama huo. Nipe upanga huo.”

10 Siku hiyo Daudi akaondoka na kuendelea kumkimbia^c Sauli, hatimaye akafika kwa Mfalme Akishi wa Gathi.^d

11 Watumishi wa Akishi wakamuuliza Akishi: “Je, huyu si Daudi mfalme wa ile nchi? Je, si yeye waliyeimba kumhusu walipocheza dansi, wakisema,

‘Sauli ameau maelfu yake, Na Daudi makumi yake ya maelfu?’^e

12 Daudi akayaweka maneno hayo moyoni mwake, naye akamwogopa sana^f Mfalme Akishi wa Gathi. **13** Kwa hiyo akajifanya hana akili timamu^g mbele yao na kutenda kama mwenda wazimu kati yao.* Alikuwa akitia alama kwenye milango ya lango na kuacha mate yake yatiririke kwenye ndevu zake. **14** Mwishowe Akishi akawaambia watumishi wake: “Hamwoni kwamba mtu huyu ni mwenda wazimu? Kwa nini mmemleta kwangu? **15** Je, nimepungukiwa na wenda wazimu hivi kwamba nahitaji mtu huyu atende kiwazimu mbele yangu? Kwa nini ameingia nyumbani mwangu?”

22 Basi Daudi akaondoka huko^h na kukimbilia katika pango la Adulamu.ⁱ Ndugu zake na nyumba yote ya baba yake waliposikia habari

21:9 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”
21:13 *Tnn., “mikononi mwao.”

hiyo, wakashuka na kumfuata huko. **2** Na watu wote walio kuwa na shida na madeni na malalamishi* wakakusanyika kwake, akawa kiongozi wao. Watu 400 hivi walikuwa pamoja naye.

3 Baadaye Daudi akaondoka huko na kwenda Misphe kule Moabu na kumwambia hivi mfalme wa Moabu:^a “Tafadhali mruhusu baba yangu na mama yangu wakae pamoja nawe mpaka nitakapojua Mungu atanifanyia nini.” **4** Basi akawaacha wakae na mfalme wa Moabu, nao wakakaa naye muda wote ambao Daudi alikuwa ndani ya ngome.^b

5 Baada ya muda nabii Gadi^c akamwambia Daudi: “Usikae ndani ya ngome. Ondoka humo uende katika nchi ya Yuda.”^d Kwa hiyo Daudi akaondoka na kwenda katika msitu wa Herethi.

6 Sauli akasikia kwamba Daudi na watu waliokuwa pamoja naye wameonekana. Wakati huo Sauli alikuwa ameketi kwenye kilima chini ya mti wa mwesheli kule Gibeaa^e akiwa ameshika mkuki wake mkononi, na watumishi wake wote walikuwa wamemzunguka. **7** Ndipo Sauli akawaambia watumishi wake walio kuwa wamemzunguka: “Tafadhali sikilizeni, enyi Wabenjamini. Je, mwana wa Yese^f atawapa ninyi nyote pia mashamba na mashamba ya mizabibu? Je, atawaweka nyote kuwa wakuu wa melfu na wakuu wa mamia?”^g **8** Ninyi nyote mmepanga njama dhidi yangu! Hakuna yeyote aliyeni-

22:2 *Au “walio kuwa na uchungu nafsini.”

SURA YA 22

a Ru 4:10, 17
1Sa 14:47

b 1Sa 22:1

c 2Sa 24:11, 12
1Nya 21:9, 10
1Nya 29:29
2Nya 29:25

d 1Sa 23:3

e 1Sa 10:26

f Ru 4:22

g 1Sa 8:11, 12

Safu ya 2

a 1Sa 18:3
1Sa 20:17

b 1Sa 21:1, 7
Zb 52:Uta

c Zb 52:2, 3

d 1Sa 14:3
1Sa 22:20

e 1Sa 21:6, 9

f 1Sa 19:4
1Sa 20:32
1Sa 24:11
1Sa 26:23

g 1Sa 17:25
1Sa 18:27

h 1Sa 18:5, 13

Julisha wakati mwana wangu mwenyewe alipofanya agano na mwana wa Yese!^a Hakuna yeyote kati yenu anayenihurumia na kunijulisha kwamba mwanangu mwenyewe amemchochea mtumishi wangu mwenyewe dhidi yangu ili anivizie, kama hali ilivyo sasa.”

9 Kisha Doegi^b Mwedomu, aliyekuwa hapo akiwa msimamizi wa watumishi wa Sauli, akamjibu hivi:^c “Nili mwona mwana wa Yese aki ja Nobu kwa Ahimeleki mwana wa Ahitubu.^d **10** Naye akamwomba Daudi mwongozo kutoka kwa Yehova na kumpa vyakula. Hata alimpa upanga wa Goliathi yule Mfilisti.”^e **11** Mara moja mfalme akaagiza Ahimeleki mwana wa kuhani Ahitubu na makuhani wote wa nyumba ya baba yake waliokuwa Nobu waitwe. Basi wote wakaja kwa mfalme.

12 Sasa Sauli akasema: “Sikiliza, tafadhali, wewe mwana wa Ahitubu!” naye akajibu: “Naam, bwana wangu.”

13 Sauli akamwambia: “Kwa nini mmepanga njama dhidi yangu, wewe na mwana wa Yese, kwa kumpa mikate na upanga na kumtafutia mwongozo kutoka kwa Mungu? Yeye hunipinga na kunivizia, kama anavyofanya sasa.”

14 Ndipo Ahimeleki akamjibu hivi mfalme: “Ni nani kati ya watumishi wako wote anayeaminika* kama Daudi?^f Yeye ni mkwe wako^g mfalme na mkuu wa walinzi wako na anahe shimika katika nyumba yako.^h

15 Je, unafikiri kwamba leo ndio mara ya kwanza kwangu kumtafutia mwongozo kutoka

22:14 *Au “aliye mwaminifu.”

kwa Mungu?^a Jambo unalosema, ni jambo nisiloweza kamwe kuwazia! Nakusihi mfalme usinikasirikie mimi mtumishi wako na nyumba yote ya baba yangu, kwa maana mimi mtumishi wako sikujua lolote kati ya mambo haya.”^b

16 Lakini mfalme akasema: “Hakika utakufa^c Ahimeleki, wewe pamoja na nyumba yote ya baba yako.”^d **17** Ndipo mfalme akawaambia wali-nzi* waliomzunguka: “Geukeni na kuwaua makuhani wa Yehova, kwa sababu wame-muunga mkono Daudi! Wali-jua kwamba ametoroka, lakini hakunijulisha!” Lakini watumishi hao wa mfalme hawakutaka kuinua mikono yao wawashambulie makuhani wa Yehova. **18** Basi mfalme akamwambia Doegi:^e “Wewe geuka uwashambulie makuhani!” Mara moja Doegi Mwedomu^f akageuka na kuwashambulia hao makuhani yeye mwenyewe. Siku hiyo aliwaua wanaume 85 waliovaa efodi ya kitani.^g **19** Pia, akalishambulia kwa upanga jiji la Nobu,^h jiji la makuhani; aliwaua kwa upanga wanaume na wanawake, watoto wadogo na wale wanaonyonya, ng’ombe dume, punda, na kondoo.

20 Hata hivyo, mwana mmoja wa Ahimeleki mwana wa Ahitubu, aliyeitwa Abiathari,ⁱ akatoroka, akakimbia kumfuata Daudi. **21** Abiathari akamwambia hivi Daudi: “Sauli amewaua makuhani wa Yehova.” **22** Ndipo Daudi akamwambia Abiathari: “Siku ile,^j Doegi Mwedomu alipokuwa huko, nilijua kwa hakika

22:17 *Tnn., “wakimbiaji.”

SURA YA 22

a 1Sa 22:10

b 1Sa 21:1, 2

c 1Sa 14:44
1Sa 20:31

d 1Sa 2:27, 32

e Zb 52:Uta

f Mwa 25:30

g 1Sa 2:27, 31

h 1Sa 21:1
1Sa 22:9i 1Sa 23:6
1Sa 30:7
2Sa 20:25
1Fa 2:27

j 1Sa 21:1, 7

Safu ya 2

a 1Fa 2:26

SURA YA 23

b Yos 15:20, 44

c 1Sa 30:8
2Sa 5:19
Zb 37:5

d 1Sa 22:5

e 1Sa 13:5
1Sa 14:52

f Amu 6:39

g 1Sa 14:6
2Sa 5:19

h 1Sa 23:1

i 1Sa 22:20

j 1Sa 23:14

kwamba atamwambia Sauli. Mimi binafsi ninawajibika kwa sababu ya kifo cha kila mtu* katika nyumba ya baba yako. **23** Kaa pamoja nami. Usiogope, kwa kuwa yeyote anayetafuta uhai wako* anatafuta uhai wangu;# nitakulinda.”^a

23 Baada ya muda Daudi aliambiwa hivi: “Wafilisti wanashambulia Keila,^b nao wanapora nafaka kwenye viwanja vya kupuria.” **2** Basi Daudi akamuuliza Yehova:^c “Je, niende nikawaue Wafilisti hawa?” Yehova akamwambia Daudi: “Nenda, waue Wafilisti hao na kuokoa Keila.” **3** Lakini wanaume wa Daudi wakamwambia: “Tazama! Ikiwa tunaogopa tukiwa hapa Yuda,^d itakuwaje tukienda Keila kupigana na vikosi vya Wafilisti?”^e **4** Kwa hiyo Daudi akamwomba tena Yehova ushauri.^f Sasa Yehova akamjibu hivi: “Ondoka, ushuke kwenda Keila kwa sababu nitawatia Wafilisti mikononi mwako.”^g **5** Basi Daudi akaenda na wanaume wake Keila na kupigana na Wafilisti; akachukua mifugo yao na kuwaua Wafilisti wengi sana, Daudi akawaokoa wakaaji wa Keila.^h

6 Sasa Abiathariⁱ mwana wa Ahimeleki alipokimbia kwenda kwa Daudi huko Keila, alikuwa na efodi. **7** Sauli akaambiwa hivi: “Daudi amekuja Keila.” Sauli akasema: “Mungu amemtia mikononi mwangu,^{*j} kwa maana amejiingiza mwenyewe ndani ya mtego kwa kuingia katika jiji lenye milango na

22:22 *Au “kila nafsi.” 22:23 *Au “nafsi yako.” #Au “nafsi yangu.” 23:7 *Tnn., “amemuza mikononi mwangu.”

makomeo.” **8** Kwa hiyo Sauli akawakusanya watu wote waende vitani, washuke Keila na kumzingira Daudi na wanaume wake. **9** Daudi alipopata habari kwamba Sauli alikuwa akipanga njama dhidi yake, akamwambia kuhani Abiathari: “Ilete efodi hapa.”^a **10** Kisha Daudi akasema: “Ee Yehova Mungu wa Israeli, mimi mtumishi wako nimesikia kwa hakika kwamba Sauli anakusudia kuja Keila kuliangamiza jiji hili kwa sababu yangu.”^b **11** Je, viongozi* wa Keila watanitia mikononi mwake? Je, Sauli atashuka kuja hapa kama mimi mtumishi wako nilivyosikia? Ee Yehova Mungu wa Israeli, tafadhali nijulishe mimi mtumishi wako.” Ndipo Yehova akamwambia: “Atashuka.” **12** Daudi akauliza: “Je, viongozi wa Keila watanitia mimi na wanaume wangu mikononi mwa Sauli?” Yehova akajibu: “Watakutia mikononi mwake.” **13** Mara moja Daudi akainuka pamoja na wanaume wake, wapatao 600,^c wakandoka Keila na kwenda popote walipoweza kwenda. Sauli alipoambiwa kwamba Daudi ametoroka Keila, hakumfuatia. **14** Daudi akakaa nyikani katika sehemu ambazo hazifikiki kwa urahisi, kwenye eneo lenye milima katika nyika ya Zifu.^d Sauli aliendelea kumtafuta,^e lakini Yehova hakumtia Daudi mikononi mwake. **15** Daudi alijua kwamba* Sauli alikuwa akimtafu-

23:11 *Au labda, “wamiliki wa masha-mba.” 23:15 *Au labda, “Daudi aliogopa kwa sababu.”

SURA YA 23

a Hes 27:21
1Sa 30:7

b 1Sa 22:19

c 1Sa 22:1, 2
1Sa 25:13
1Sa 30:9

d Yos 15:20, 55
1Sa 23:19
1Sa 26:1

e 1Sa 18:29
1Sa 20:33
1Sa 27:1

Safu ya 2

a Zb 37:5
Met 17:17

b 1Sa 16:13
2Sa 2:4
2Sa 5:3

c 1Sa 20:31
1Sa 24:17, 20

d 1Sa 18:3
1Sa 20:42

e 1Sa 10:26

f 1Sa 26:1
Zb 54:Uta

g 1Sa 23:15

h 1Sa 26:3

i 1Sa 23:24

j Zb 54:3

ta ili amue* Daudi alipokuwa katika nyika ya Zifu huko Horeshi.

16 Sasa Yonathani mwana wa Sauli akaenda kumwona Daudi huko Horeshi, akamsaidia kupata nguvu* katika Yehova.^a **17** Akamwambia: “Usiogope, kwa maana Sauli baba yangu hatakupata; utakuwa mfalme wa Israeli,^b nami nitakuwa wa pili baada yako; na Sauli baba yangu anajua jambo hilo.”^c **18** Kisha wote wawili wakafanya agano^d mbele za Yehova, na Daudi akaendelea kukaa Horeshi, naye Yonathani akaenda nyumbani kwake.

19 Baadaye watu wa Zifu wakapanda kwenda kwa Sauli kule Gibe^e na kumwambia: “Daudi anajificha karibu nasi^f katika sehemu ambazo hazifikiki kwa urahisi kule Horeshi,^g kwenye kilima cha Hakila,^h kilicho upande wa kusini* wa Yeshimoni.”ⁱ **20** Wakati wowote utakaopenda kushuka huko, Ee mfalme, shuka, nasi tutamtia mikononi mwako mfalme.”^j **21** Ndipo Sauli akasema: “Yehova na awabariki kwa sababu mmenihurumia. **22** Tafadhali nendeni mjaribu kutafuta mahali hususa alipo na mtu aliyemwona huko, kwa sababu nimeambiwa kwamba yeye ni mjanja sana. **23** Chunguzeni kwa makini kila mahali anapojificha na mrudi kwangu mkiwa na ushahidi. Kisha nitaenda pamoja nanyi, na ikiwa yuko

23:15 *Au “alikuwa akiitafuta nafsi yake.” 23:16 *Tnn., “akauimarisha mkono wake.” 23:19 *Tnn., “upande wa kulia.” #Au labda, “wa jangwa; nyika.”

nchini, nitamsaka kabisa miongoni mwa maelfu yote ya* Yuda.”

24 Basi wakaondoka na kumtangulia Sauli kwenda Zifu,^a na wakati huo Daudi na wanaume wake walikuwa katika nyika ya Maoni,^b kule Araba^c upande wa kusini wa Yeshimoni. **25** Kisha Sauli akaja na wanaume wake kumtafuta.^d Daudi alipoambiwa jambo hilo, akashuka mara moja na kwenda kwenye mwamba,^e naye akakaa katika nyika ya Maoni. Sauli aliposikia hilo, akamfuatia Daudi katika nyika ya Maoni. **26** Sauli alipofika upande mmoja wa mlima, Daudi na wanaume wake walikuwa upande wa pili wa mlima huo. Daudi alikuwa akifanya haraka kumkimbia^f Sauli, lakini Sauli na wanaume wake walikuwa wakimkaribia Daudi na wanaume wake ili wawakamate.^g **27** Lakini mjumbe fulani akaja kwa Sauli na kumwambia: “Njoo haraka, kwa sababu Wafilisti wameivamia nchi!” **28** Ndipo Sauli akacha kumfuatia Daudi,^h akienda kukabiliana na Wafilisti. Ndiyo sababu mahali hapo paliitwa Mwamba wa Migawanyiko.

29 Kisha Daudi akapanda kutoka huko na kwenda kukaa katika sehemu ambazo hazifikiki kwa urahisi kule En-gedi.ⁱ

24 Mara tu Sauli aliporudi baada ya kuwafuatia Wafilisti, aliambiwa hivi: “Tazama! Daudi yuko katika nyika ya En-gedi.”^j

2 Basi Sauli akachukua wanaume 3,000 mashujaa kutoka nchi yote ya Israeli na kwenda

SURA YA 23

a 1Sa 23:14

b Yos 15:20, 55
1Sa 25:2, 3

c Kum 1:7

d 1Sa 26:2
Zb 54:3

e 1Sa 23:28

f Zb 31:22

g Zb 17:9

h Zb 54:7

i Yos 15:20, 62
Wim 1:14

SURA YA 24

j 1Sa 23:28, 29

Safu ya 2

a Zb 57:Uta
Zb 142:Uta

b 1Sa 26:8, 23

c 2Sa 24:10

d Kut 22:28
1Sa 26:11
2Sa 1:14
1Nya 16:22

e 1Sa 26:17

kumtafuta Daudi na wanaume wake kwenye miamba ya mbuzi wa milimani. **3** Sauli akafika kwenye mazizi ya kondoo yaliyojengwa kwa mawe kando ya barabara, mahali ambapo palikuwa na pango, akaingia pangoni kwenda haja,* wakati huo Daudi na wanaume wake walikuwa wameketi ndani kabisa ya pango hilo.^a **4** Wanaume wa Daudi wakamwambia: “Hii ndiyo siku ambayo Yehova anakwambia, ‘Tazama! Ninamtia adui yako mikononi mwako,^b nawe unaweza kumtendea jambo lolote unalotaka.’” Kwa hiyo Daudi akasimama, akakata kikyakimya upindo wa joho la Sauli lisilo na mikono. **5** Lakini baadaye moyo wa Daudi ukaendelea kumchoma*^c kwa sababu alikuwa amekata upindo wa joho la Sauli lisilo na mikono. **6** Akawaambia wanaume wake: “Siwezi kamwe kuwazia, kulingana na maoni ya Yehova, kumtendea jambo kama hilo bwana wangu, mtiwa-mafuta wa Yehova, kwa kuinua mkono wangu dhidi yake, kwa kuwa yeye ni mtiwa-mafuta wa Yehova.”^d **7** Basi Daudi akawazulia* wanaume wake kwa maneno hayo, naye hakuwaruhusu wamshambuliye Sauli. Sauli akaondoka pangoni na kwenda zake.

8 Baadaye Daudi akainuka na kutoka pangoni, akamwita Sauli: “Bwana wangu mfalme!”^e Sauli alipoangalia nyuma, Daudi aliinama hadi chini kifudifudi na kusujudu. **9** Daudi akamuuliza Sauli:

24:3 *Tnn., “afunike miguu yake.” **24:5**

*Au “dhamiri ya Daudi ikaendelea kumchoma.” **24:7** *Au labda, “akawatawanya.”

"Kwa nini unasikiliza maneno ya watu wanaosema, "Tazama! Daudi anataka kukudhuru"?^a **10** Siku hii ya leo umeona kwa macho yako mwenyewe jinsi Yehova alivyokutia mikononi mwangu pangoni. Lakini mtu fulani aliposema nikuue,^b nilikusikitikia nikasema, "Sitainua mkono wangu dhidi ya bwana wangu, kwa maana yeye ni mtiwa-mafuta wa Yehova."^c **11** Tazama baba yangu, angalia nimeshika upindo wa joho lako lisilo na mikono; kwa sababu nilipokata upindo wa joho lako lisilo na mikono, sikukuu. Sasa unaweza kuona na kuelewa kwamba sikusudii kukudhuru wala kukua-si, nami sijakutendea dhambi,^d lakini wewe unaniwinda ili kunuia.*^e **12** Yehova na ahukumu kati yangu na wewe,^f na Yehova anilipizie kisasi mambo unayonitendea,^g lakini sitainua mkono wangu dhidi yako.^h **13** Kama methali ya kale inavyosema, "Kutoka kwa mwovu hutoka uovu," lakini sitainua mkono wangu dhidi yako. **14** Mfalme wa Israeli ametoka kumtafuta nani? Unamfuatia nani? Mbwa aliyekufa? Kiroboti mmoja?ⁱ **15** Yehova na awe mwamuzi, atahukumu kati yangu na wewe, naye ataona na kunitetea na kuamya kesi yangu^j na kuniokoa kutoka mikononi mwako."

16 Mara tu Daudi alipomaliza kumwambia maneno hayo, Sauli akasema: "Je, hiyo ni sauti yako, Daudi mwangu?"^k Kisha Sauli akaanza kulia kwa sauti kubwa. **17** Akamwambia Daudi: "Wewe ni mwadilifu kuliko

24:11 *Au "kuiua nafsi yangu."

SURA YA 24

a 1Sa 26:19

b 1Sa 24:4

c 1Sa 9:16
1Sa 10:1
1Sa 26:9
Zb 105:15d 1Sa 26:18
Zb 35:7

e 1Sa 23:14

f 1Sa 26:23

g Kum 32:35

h 1Sa 26:11

i 1Sa 26:20

j 1Sa 25:39
Zb 35:1

k 1Sa 26:17

Safu ya 2

a 1Sa 26:21

b 1Sa 24:4, 10

c 1Sa 26:25
Zb 18:20d 1Sa 13:14
1Sa 15:28
1Sa 18:8
1Sa 20:31
1Sa 23:17e Law 19:12
Kum 6:13f 2Sa 9:1
2Sa 21:7

g 1Sa 15:34

h 1Sa 23:29

SURA YA 25

i 1Sa 1:20
1Sa 2:18
1Sa 3:20
Zb 99:6

j 1Sa 7:15, 17

k 1Sa 23:24

l Yos 15:20, 55

m 1Sa 25:25

n 1Sa 27:3

mimi, kwa maana umenitendea mema lakini mimi nimekulipa kwa uovu.^a **18** Naam, leo umeniambia mema uliyotenda kwa kukosa kunuia Yehova aliponitia mikononi mwako.^b **19** Ni mtu gani anayempata adui yake na kumwacha aende zake bila kumdhuru? Yehova ataku-thawabisha wewe kwa mema^c kwa sababu ya mambo uliyonifanyia leo. **20** Sasa tazama! Najua kwa hakika kwamba utatawala ukiwa mfalme^d na kwamba ufalme wa Israeli utadumu mikononi mwako. **21** Sasa niapie mbele za Yehova^e kwamba hutawafagilia mbali wazao wangu* baada yangu na kwamba hutalifutia mbali jina langu kutoka katika nyumba ya baba yangu."^f **22** Kwa hiyo Daudi akamwambia Sauli, kisha Sauli akaenda nyumbani kwake.^g Lakini Daudi na wanaume wake wakapanda kwenda ndani ya ngome.^h

25 Baada ya muda Samweliⁱ akafa; na Waisraeli wote wakakusanyika pamoja kumwbolezea na kumzika nyumbani kwake huko Rama.^j Kisha Daudi akaondoka na kushuka kwenda katika nyika ya Parani.

2 Sasa kulikuwa na mtu fulani kule Maoni^k aliyekuwa akifanya kazi Karmeli.*^l Mtu huyo alikuwa tajiri sana; alikuwa na kondoo 3,000 na mbuzi 1,000, naye alikuwa akiwakata kondoo wake manyoya huko Karmeli. **3** Mtu huyo aliitwa Nabali,^m na mke wake aliitwa Abigaili.ⁿ Mke

24:21 *Tnn., "mbegu yangu." 25:2 *Jiji fulani kule Yuda; si Mlima Karmeli.

huyo alikuwa mwenye busara* na mrembo, lakini mume wake, Mkalebu,^a alikuwa mkali na mwenye tabia mbaya.^b

4 Daudi akasikia akiwa nyikani kwamba Nabali alikuwa akiwakata kondoo wake manyoya. **5** Kwa hiyo Daudi akawatuma vijana kumi wanaume waende kwa Nabali, akawaambia: "Pandeni mwennde Karmeli, na mtakapofika kwa Nabali, mjulieni hali yake kwa jina langu. **6** Kisha mwambieni, 'Uishi misha marefu na uwe na amani na nyumba yako iwe na amani na vitu vyako vyote viwe na amani. **7** Sasa nimesikia kwamba unawakata kondoo wako manyoya. Wachungaji wako walipokuwa pamoja nasi hatukuwadhuru,^c na wakati wote walipokuwa Karmeli hawakupoteza chochote. **8** Waulize vijana wako, nao watakwambia. Vijana wangu na wapate kibali machoni pako, kwa sababu tumekuja wakati wa shangwe.* Tafadhali tupatie sisi watumishi wako na Daudi mwana wako chochote unachoweza kumpa."^d

9 Basi vijana wa Daudi wakaenda na kumwambia Nabali mambo yote hayo kwa jina la Daudi. Walipomaliza, **10** Nabali akawajibu hivi watumishi wa Daudi: "Daudi ni nani, na mwana wa Yese ni nani? Siku hizi watumishi wengi wanawatoroka mabwana zao.^e **11** Ninaweza je kuchukua mikate yangu na maji yangu na nyama niliyowachinjia wakataji manyoya wangu na kuwapa

25:3 *Au "utambuzi." 25:8 *Tnn., "siku nzuri."

SURA YA 25

a Hes 13:6
Hes 32:11, 12

b 1Sa 25:17, 21

c 1Sa 25:14-16

d Kum 15:7

e 1Sa 22:2

Safu ya 2

a Zb 37:8
Met 15:1
Mhu 7:9

b 1Sa 25:10

c 1Sa 25:7

d 1Sa 25:13

e 1Sa 25:3

f 1Sa 25:3

watu ambao hata hawajulikani wanatoka wapi?"

12 Kwa hiyo vijana wa Daudi wakarudi na kumwambia Daudi maneno hayo yote. **13** Mara moja Daudi akawaambia wanaume wake: "Kila mtu ajifunge upanga wake!"^a Basi wote wakajifunga panga zao, na Daudi pia akajifunga upanga wake mwenyewe, na wanaume wapatao 400 wakapanda pamoja na Daudi, huku wanaume 200 wakibaki na mizigo.

14 Wakati huo, mtumishi mmoja akamletea Abigaili mke wa Nabali habari hii: "Tazama! Daudi aliwatuma wajuombe kutoka nyikani ili kumtaka mema bwana wetu, lakini aliwatukana vikali.^b **15** Wanaume hao walitutendea kwa wema sana. Hawakutudhuru kamwe, nasi hatukukosa hata kitu kimoja wakati wote tulipokuwa nao malishoni.^c **16** Walikuwa kama ukuta wa ulinzi kutuzunguka, usiku na mchana, wakati wote tulipokuwa nao tukichunga kondoo. **17** Sasa amua utakalofanya, kwa maana kwa hakika bwana wetu ataangamizwa pamoja na nyumba yake yote,^d naye ni mtu asiyefaa kitu* hivi^e kwamba hakuna mtu anayeweza kuzungumza naye."

18 Basi Abigaili^f akachukua haraka mikate 200, mitungi miwili mikubwa ya divai, kondoo watano waliochinjwa, sea tano* za nafaka iliyokaangwa, keki 100 za zabibu kavu, na keki 200 za tini zilizoshinikizwa, akapakia vitu hivyo

25:17 *Au "asiye na maana." 25:18 *Sea moja ilikuwa sawa na lita 7.33 (vibaba 6.66). Angalia Nyongeza B14.

vyote juu ya punda.^a **19** Ki-sha akawaambia watumishi wake: “Tangulieni; nitawafuata.” Lakini hakumwambia Nabali mumewe jambo lolote.

20 Abigaili alipokuwa juu ya punda akishuka bondeni nyuma ya mlima, alikutana kwa ghafla na Daudi na wanaume wake wakishuka kumwelekea. **21** Sasa Daudi alikuwa akisema: “Ilikuwa kazi ya bure kulinda mali yote ya mtu huyu nyikani. Haku-na kitu chake hata kimoja kilichopotea,^b lakini ananilipa uovu kwa wema niliomfanyia.^c **22** Mungu na awaadhibu, tena vikali, maadui wa Daudi* ikiwa nitamwacha mwana-mume wake yeyote^d abaki hai mpaka asubuhi.”

23 Abigaili alipomwona Daudi, alishuka haraka kutoka juu ya punda na kuanguka kifudufudi mbele ya Daudi, huku akiinama chini. **24** Ki-sha akaanguka miguuni pake na kusema: “Bwana wangu, acha nibebe lawama; niruhusu mimi kijakazi wako nizungumze nawe, na usikilize maneno ya kijakazi wako. **25** Tafadhali, bwana wangu usimsikilize huyu Nabali asiyefaa kitu,^d kwa maana jina lake linamfaa kabisa. Anaitwa Nabali,* na kwa kweli ni mtu mpumbavu. Lakini mimi kijakazi wako, si-kuwaona vijana wako bwana wangu, uliowatuma. **26** Na sasa, bwana wangu, kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kama wewe unavyoishi, Yeho-

25:22 *Au labda, “Mungu na amwadhibu Daudi, tena vikali.” ^dTnn., “mtu yeyote anayekojoa ukutani.” Huu ni msemu wa Kiebrania na kuwadharau wanaume. 25:25 *Maana yake “Mpu-mbavu; Mjinga.”

SURA YA 25

a 2Sa 16:1
2Sa 17:27-29

b 1Sa 25:7

c 1Sa 25:10
Zb 35:12

d 1Sa 25:17

Safu ya 2

a Mwa 20:6

b Mwa 9:6

c 1Sa 25:18

d 1Sa 22:2
1Sa 25:13e 1Sa 15:28
2Sa 7:8, 11
1Fa 9:5f 1Sa 17:45
1Sa 18:17g 1Sa 24:11
1Fa 15:5h 1Sa 13:13, 14
1Sa 23:17
2Sa 6:21
2Sa 7:8
Zb 89:20i Kum 32:35
1Sa 24:15

va ndiye amekuzuia^a usiwe na hatia ya damu^b na usilipize kisasi* kwa mkono wako mwenyewe. Maadui wako na wale wanaotaka kukudhuru bwana wangu na wawe kama Nabali. **27** Sasa pokea zawadi*^c hii ambayo mimi kijakazi wako nimekuletea bwana wangu na uwape vijana wanaokufuata bwana wangu.^d **28** Tafadhali, nisamehe kosa langu mimi kijakazi wako, kwa maana hakika Yehova atakujengea wewe bwana wangu nyumba inayodumu,^e kwa sababu wewe bwana wangu unapigana vita vya Yehova,^f na uovu haujaonekana ndani yako siku zako zote.^g **29** Mtu akiinuka ili akufuatie na kuatafuta uhai wako,* Yehova Mungu wako atakuwa amefungia salama uhai wako^h katika mfuko wa uzima, bwana wangu, lakini atautupa mbali uhai wa maadui wako kama mawe yanavyotupwa kwa kombeo. **30** Na baada ya Yehova kukufanyia wewe bwana wangu mambo yote mema aliyoahidi na kukuweka kuwa kiongozi wa Israeli,^h **31** hutahuzunika wala kujuta moyoni mwako kwa sababu ya kumwaga damu bila sababu na kulipiza kisasi*ⁱ kwa mkono wako bwana wangu. Yehova atakapokutenda mema bwana wangu, nikumbuke mimi kijakazi wako.”

32 Ndipo Daudi akamwambia Abigaili: “Msifu Yehova Mungu wa Israeli, aliyekutumama leo ukutane nami! **33** Busara yako na ibarikiwe! Na ubarikiwe kwa kunizuia leo

25:26 *Au “usiokoe.” 25:27 *Tnn., “baraka.” 25:29 *Au “kutatfuta nafsi yako.” ^dAu “nafsi yako.” 25:31 *Au “kuokoa.”

nisiwe na hatia ya damu^a na nisilipize kisasi* kwa mikono yangu mwenyewe. **34** La si- vyo, kwa hakika kama Yehova Mungu wa Israeli anavyoi- shi aliyenizua nisikudhuru,^b ikiwa hungekuja haraka ku- kutana nami,^c kufikia asubu- hi hakuna mwanamume hata mmoja* wa Nabali angekuwa hai.”^d **35** Basi Daudi akapo- kea vitu ambavyo Abigaili ali- kuwa amemletea na kumwa- mbia: “Panda uende nyumba- ni kwako kwa amani. Tazama, nimekusikiliza na nitatimiza ombi lako.”

36 Baadaye Abigaili akaru- di kwa Nabali, naye Nabali ali- kuwa akila na kunywa kama mfalme nyumbani mwake, na alikuwa amechangamka sana* na kulewa kabisa. Lakini Abi- gaili hakumwambia jambo lolote mpaka asubuhi kulipo- pambazuka. **37** Asubuhi, di- vai ilipokuwa imemtoka Na- bali, mke wake akamwambia mambo hayo. Na moyo wa Na- bali ukawa kama wa mtu aliye- kufa, akalala akiwa amepoo- za kama jiwe. **38** Siku kumi hivi baadaye, Yehova akampi- ga Nabali, naye akafa.

39 Daudi aliposikia kwa- mba Nabali amekufa, akase- ma: “Asifiwe Yehova, ambaye amenitetea^e baada ya kuaibi- shwa na Nabali,^f na amenizua mimi mtumishi wake nisi- tende jambo lolote ovu,^g na Yehova amemwadhibu Nabali kwa sababu ya uovu wake!”*

25:33 *Au “nisiokoe.” 25:34 *Tnn., “mtu yeyote anayekojoa ukutani.” Huu ni msemu wa Kiebrania wa kuwadha- rau wanaume. 25:36 *Tnn., “moyo wa Nabali ulikuwa umechangamka sana.” 25:39 *Tnn., “amerudisha uovu wa Na- bali juu ya kichwa chake mwenyewe!”

SURA YA 25

a Kum 19:10
1Sa 25:26

b 1Sa 25:24

c 1Sa 25:18

d 1Sa 25:22

e 1Sa 24:15
Zb 35:1

f 1Sa 25:10, 14

g 1Sa 25:34

Safu ya 2

a Mwa 18:3, 4
Lu 7:44

b 1Sa 25:3

c 1Sa 27:3
2Sa 3:2
1Nya 3:1

d Yos 15:20, 56

e 1Sa 30:5
2Sa 5:13

f 1Sa 18:20

g 2Sa 3:14, 15

SURA YA 26

h Yos 15:20, 55

i Amu 19:14
1Sa 10:26j 1Sa 23:14
1Sa 23:19, 24
Zb 54:Uta

k 1Sa 24:2

Kisha Daudi akawatuma wa- jumbe kwa Abigaili akio- mba awe mke wake. **40** Basi watumishi wa Daudi wakafika kwa Abigaili huko Karmeli na kumwambia: “Daudi ametutu- ma kwako ili tukuchukue uwe mke wake.” **41** Mara moja akasimama na kuinama chini kifudifudi na kusema: “Nipo hapa mimi mtumwa wako, ili niwe kijakazi wa kuwaosha miguu^a watumishi wa bwana wangu.” **42** Kisha Abigaili^b akasimama haraka na kupan- da juu ya punda wake na vija- kazi wake watano walitembea nyuma yake; alienda pamo- ja na wajumbe wa Daudi, aka- wa mke wake.

43 Daudi alikuwa pia ame- mwoa Ahinoamu^c kutoka Yez- reeli,^d na wanawake wote wa- wili wakawa wake zake.^e

44 Lakini Sauli alikuwa amemchukua Mikali binti yake,^f mke wa Daudi na ku- mpa Palti^g mwana wa Laishi, kutoka Galimu.

26 Baada ya muda watu wa Zifu^h wakaja kwa Sauli huko Gibeai,ⁱ wakisema: “Dau- di amejificha kwenye kilima cha Hakila, ng’ambo ya Yeshi- moni.”*^j **2** Basi Sauli akaon- doka na kushuka kwenda ka- tika nyika ya Zifu akiwa na wanaume 3,000 mashujaa wa Israeli ili kumtafuta Daudi ka- tika nyika ya Zifu.^k **3** Sauli akapiga kambi kwenye kilima cha Hakila, kilicho ng’ambo ya Yeshimoni, kando ya bara- bara. Wakati huo Daudi ali- kuwa akiishi nyikani, akapata habari kwamba Sauli aliku- wa amekuwa nyikani kumta- futa. **4** Basi Daudi akatuma

26:1 *Au labda, “jangwa; nyika.”

wapelelezi ili wathibitische kwamba kwa kweli Sauli alikuwa amekuja. **5** Baadaye Daudi akaenda mahali ambapo Sauli alikuwa amepiga kambi, na Daudi akaona mahali ambapo Sauli na Abneri^a mwana wa Neri, mkuu wa jeshi lake, walikuwa wamelala; Sauli alikuwa amelala ndani ya kambi akiwa amezunguka na wanajeshi. **6** Kisha Daudi akamuuliza hivi Ahimeleki Mhiti^b na Abishai^c mwana wa Seruya,^d ndugu ya Yoabu: “Ni nani atakayeshuka pamoja nami kwenda kwa Sauli kambini?” Abishai akajibu: “Mimi nitashuka pamoja nawe.” **7** Basi Daudi na Abishai wakaenda kwa jeshi hilo usiku, wakamkuta Sauli amelala ndani ya kambi mkuki wake ukiwa umedungwa ardhini karibu na kichwa chake; Abneri na wanajeshi walikuwa wamelala kumzunguka Sauli.

8 Ndipo Abishai akamwambia Daudi: “Leo Mungu ametmbia adui yako mikononi mwako.^e Na sasa tafadhali, acha nimpigilie ardhini kwa mkuki mara moja tu, wala sitafanya hivyo mara mbili.” **9** Hata hivyo, Daudi akamwambia Abishai: “Usimdhuru, kwa maana ni nani anayeweza kuinua mkono wake dhidi ya mtiwamafuta wa Yehova^f na asiwe na hatia?”^g **10** Daudi akaendelea kusema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, Yehova mwenyewe atampiga,^h au siku yake itafikaⁱ naye ataku fa, au ataenda vitani na kuuawa.^j **11** Ni jambo nisiloweza kamwe kuwazia, kulingana na maoni ya Yehova, kwamba ninue mkono wangu dhidi ya

SURA YA 26

a 1Sa 14:50
1Sa 17:55
2Sa 2:8
2Sa 3:27

b Mwa 10:15

c 2Sa 16:9
2Sa 18:5
2Sa 23:18

d 2Sa 2:18
1Nya 2:15, 16

e 1Sa 24:4
1Sa 26:23

f 1Sa 10:1

g 1Sa 24:6
2Sa 1:14
1Nya 16:22
Zb 20:6

h Kum 32:35
1Sa 24:12
1Sa 25:38
Zb 94:1, 23

i Zb 37:12, 13

j 1Sa 31:3, 6

Safu ya 2

a Law 19:18
1Sa 24:6
1Nya 16:22
Zb 105:15

b 1Sa 24:4

c 1Sa 14:50
1Sa 17:55
2Sa 2:8
2Sa 3:8

d 1Sa 26:8

e 1Sa 9:16, 17
1Sa 10:1

f 1Sa 26:11

g 1Sa 24:8, 16

mtiwa-mafuta wa Yehova!^a Sasa, tafadhali, chukua huo mkuki ulio karibu na kichwa chake na hilo gudulia la maji, twende zetu.” **12** Basi Daudi akachukua mkuki na gudulia la maji karibu na kichwa cha Sauli, wakaenda zao. Hakuna yeyote aliyejua wala kuwao-na^b wala kuamka, kwa maana wote walikuwa wamelala, kwa sababu walikuwa wame-shikwa na usingizi mzito kutoka kwa Yehova. **13** Kisha Daudi akavuka ng’ambo na kusimama juu ya mlima uliokuwa umbali fulani kutoka kwenye kambi ya Sauli.

14 Daudi akawaita kwa sauti wanajeshi hao na Abneri^c mwana wa Neri, akisema: “Abneri, unanisikia?” Abneri akajibu: “Wewe ni nani unayemwita mfalme?” **15** Daudi akamwambia Abneri: “Je, wewe si mwanamume? Na ni nani aliye kama wewe katika hukumu Israeli? Kwa nini basi hukumlinda bwana wako mfalme? Kwa sababu mwanajeshi mmoja aliingia kambini ili kumwagamiza bwana wako mfalme.^d **16** Jambo ulilofanya si zuri. Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, mnastahili kufa, kwa sababu hamkuendelea kumlinda bwana wenu, mtiwa-mafuta wa Yehova.^e Sasa angalia kila mahali! Uko wapi mkuki wa mfalme na gudulia la maji^f lililokuwa karibu na kichwa chake?”

17 Ndipo Sauli akaitambua sauti ya Daudi na kumuuliza: “Je, hiyo ni sauti yako mwangu Daudi?”^g Daudi akajibu: “Ni sauti yangu, bwana wangu mfalme.” **18** Halafu akaendelea kusema: “Bwana wangu kwa nini unanifua-

tia mimi mtumishi wako,^a ni-mefanya nini, nami nina ha-tia ya kosa gani?^b **19** Tafa-dhali, bwana wangu mfalme, yasikilize maneno yangu mimi mtumishi wako: Ikiwa ni Ye-hova aliyekuchocha dhidi ya-nangu, acha akubali* toleo lan-gu la nafaka. Lakini ikiwa ni wanadamu wamekuchochea,^c wamelaaniwa mbele za Yehova, kwa sababu leo wamenifu-kuza ili nisiungane na urithi wa Yehova,^d wakisema, 'Nenda, abudu miungu mingine!' **20** Na sasa usiache damu yan-gu imwagike ardhini mbali kutoka mbele za* Yehova, kwa maana mfalme wa Israeli ame-toka kwenda kutafuta kirobo-to mmoja,^e kama mtu anayewi-nda kware milimani."

21 Ndipo Sauli akasema: "Nimetenda dhambi.^f Rudi, mwanangu Daudi, kwa maana sitakudhuru tena, kwa sababu umeona uhai wangu kuwa we-nye* thamani^g leo. Naam, ni-metenda kipumbavu, nami ni-mekosea sana." **22** Daudi akamwambia: "Mkuki wa mfa-lme ndio huu. Mruhusu mmo-ja wa vijana wako aje kuuchua. **23** Yehova ndiye ataka-yemlipa kila mtu kulingana na uadilifu wake mwenyewe^h na uaminifu wake mwenyewe, kwa kuwa leo Yehova alikutia mikononi mwangu, lakini si-kutaka kuinua mkono wangu dhidi ya mtiwa-mafuta wa Ye-hova.ⁱ **24** Tazama! Kama ni-livyoona uhai wako kuwa we-nye* thamani leo, uhai wa-n-gu na uwe wenye^g thama-

26:19 *Tnn., "anuse." 26:20 *Au "ku-toka kwenye uwepo wa." 26:21 *Au "umeona nafsi yangu kuwa yenye." 26:24 *Au "nafsi yako kuwa yenye." ^aAu "nafsi yangu na iwe yenye."

SURA YA 26

a Zb 35:7

b 1Sa 24:9, 11

c 1Sa 24:9

d Kut 19:5
Kum 26:18

e 1Sa 24:14

f 1Sa 24:17

g 1Sa 24:10
1Sa 26:11h Zb 7:8
Zb 18:20i 1Sa 24:6
1Sa 26:9

Safu ya 2

a Zb 34:19

b 1Sa 24:19

c 1Sa 24:22
1Sa 27:4

SURA YA 27

d 1Sa 19:18
1Sa 22:1, 5e 1Sa 18:29
1Sa 23:23f 1Sa 25:13
1Sa 30:9g 1Sa 21:10, 14
1Sa 27:12

h 1Sa 25:43

i 1Sa 25:39, 42

j 1Sa 23:14
1Sa 26:25k Yos 19:1, 5
1Sa 30:1
2Sa 1:1
1Nya 12:1, 20

ni machoni pa Yehova, na aniokoe kutoka katika mate-so yote."^a **25** Sauli akamwa-mbia Daudi: "Ubarikiwe, mwa-nangu Daudi. Hakika utatenda mambo makubwa, na ha-kika utashinda."^b Kisha Daudi akaenda zake, na Sauli akaru-di kwake.^c

27 Hata hivyo, Daudi aka-sema moyoni mwake: "Siku moja mkono wa Sauli utaniau. Jambo bora la kufanya ni kukimbilia^d nchi wa Wa-filisti; halafu Sauli ataka-ta tamaa ya kunitafuta kati-ka eneo lote la Israeli,^e nami nitaponyoka kutoka mkono-ni mwake." **2** Basi Daudi akaondoka pamoja na wanau-me 600^f waliokuwa naye, akavuka kwenda kwa Aki-shi^g mwana wa Maoki, mfal-me wa Gathi. **3** Daudi na wa-naume wake wakakaa na Aki-shi huko Gathi, kila mwana-mume na familia yake. Daudi alikuwa na wake zake wawili, Ahinoamu^h wa Yezreeli na Abigailiⁱ Mkarmeli, mjane wa Nabali. **4** Sauli alipoambiwa kwamba Daudi alikuwa ame-kimbia kwenda Gathi, aliacha kumtafuta.^j

5 Ndipo Daudi akamwambia Akishi: "Ikiwa nimepata ki-bali machoni pako, naomba unipe mahali katika mojawapo ya majiji ya mashambani, ili niishi huko. Kwa nini mimi mtumishi wako niishi pamoja nawe katika jiji hili la kifal-me?" **6** Basi Akishi akampa Siklagi^k siku hiyo. Ndiyo sababu tangu siku hiyo Sikla-gi limekuwa jiji la wafalme wa Yuda.

7 Daudi aliishi katika eneo la mashambani la Wafilisti kwa muda wa mwaka mmoja

na miezi minne.^a **8** Daudi alikuwa akipanda pamoja na wanaume wake kuwavamia Wageshuri,^b Wagirzi, na Waamaleki,^c kwa maana walikuwa wakikaa katika nchi iliyoanzia Telamu mpaka Shuri^d na kushuka mpaka nchi ya Misiri. **9** Daudi alipokuwa akishambulia nchi, hakumwacha hai mwanamume wala mwanamke yeyote,^e bali alichukua kondoo, ng'ombe, punda, ngamia, na mavazi, kisha alirudi kwa Akishi. **10** Na Akishi alipokuwa akimuuliza: "Ulivamia wapi leo?" Daudi alimjibu: "Upande wa kusini wa* Yuda"^f au "Upande wa kusini wa Wayerahmeeli"^g au "Upande wa kusini wa Wakeni."^h **11** Daudi hakumwacha hai mwanamume au mwanamke yeyote ili wasiletwe Gathi, kwa kuwa alisema: "Wasije wakawaambia habari zetu wakisema, 'Hivi ndivyo Daudi alivyofanya.'" (Alizoea kufanya hivyo muda wote alioishi katika eneo la mashambani la Wafilisti.) **12** Kwa hiyo Akishi akamwamini Daudi akisema moyoni mwake: "Bila shaka ananuka miongoni mwa watu wake wa Israeli, kwa hiyo atakuwa mtumishi wangu sikuzote."

28 Siku hizi Wafilisti walikusanya majeshi yao kwenda kupigana vita na Waisraeli.ⁱ Basi Akishi akamwambia Daudi: "Bila shaka unajua kwamba wewe na wanaume wako mtaenda pamoja nami vitani."^j **2** Kwa hiyo Daudi akamwambia Akishi: "Kwa hakika unajua jambo ambalo mimi mtumishi wako nitafanya." Akishi akamwa-

27:10 *Au "Dhidi ya Negebu ya."

SURA YA 27

a 1Sa 29:3

b Yos 13:1, 2

c Mwa 36:12
Kut 17:8, 14
Hes 13:29
1Sa 15:2
2Sa 1:1d Mwa 25:17, 18
Kut 15:22
1Sa 15:7e Kum 25:19
1Sa 15:3

f Yos 15:1, 2

g 1Nya 2:9

h Hes 24:21
1Sa 15:6

SURA YA 28

i 1Sa 14:52

j 1Sa 27:12
1Sa 29:3

Safu ya 2

a 1Sa 29:2

b 1Sa 25:1

c Kut 22:18
Law 19:31
Law 20:6, 27
Kum 18:10, 11
Ufu 21:8d Yos 19:17, 18
2Fa 4:8e 1Sa 31:1
2Sa 1:21
2Sa 21:12

f 1Sa 28:20

g 1Sa 14:37

h Kut 28:30
Hes 27:21i Kut 22:18
Law 19:31
Law 20:6
1Sa 15:23
1Sa 28:3

j Yos 17:11

k Kum 18:10, 11
1Nya 10:13

mbia Daudi: "Ndiyo sababu nitakuweka kuwa mlinzi wangu wa kudumu."*^a

3 Wakati huo Samweli alikuwa amekufa, na Waisraeli wote walikuwa wamemwbolezea na kumzika katika jiji lake mwenyewe la Rama.^b Naye Sauli alikuwa amewaoondoa nchini watu wanaowasiliana na roho na pia wabashiri.^c

4 Wafilisti wakakusanyika na kwenda kupiga kambi Shunemu.^d Basi Sauli akawakusanya Waisraeli wote, nao wakapiga kambi Gilboa.^e **5** Sauli alipoona kambi ya Wafilisti, akaogopa, na moyo wake ukatetemeka sana.^f **6** Ingawa Sauli alikuwa akimwomba Yehova ushauri,^g Yehova hakumjibu kamwe, iwe ni katika ndoto au kwa Urimu^h au kupitia manabii. **7** Hatimaye Sauli akawaambia watumishi wake: "Nitafutieni mwanamke anayewasiliana na roho,ⁱ nitaenda kwake kumwomba ushauri." Watumishi wake wakamwambia: "Tazama! Kuna mwanamke anayewasiliana na roho kule Endori."^j

8 Kwa hiyo Sauli akaficha sura yake, akavaa mavazi mengine na kwenda kwa mwanamke huyo usiku akiwa na wanaume wake wawili. Akasema: "Tafadhali, nifanyie uaguzi* kwa kuwasiliana na roho,^k nikipandishie yule nitakayekutajia." **9** Hata hivyo, mwanamke huyo akamwambia: "Unajua vizuri mambo ambayo Sauli alifanya, jinsi alivyo waondoa nchini watu wanao-

28:2 *Tnn., "kuwa mlinzi wa kichwa changu siku zote." 28:8 *Au "nibashirie."

wasiliana na roho na pia wabashiri.^a Kwa nini basi unajaribu kunitega ili niuawe?”^b

10 Ndipo Sauli akamwambia kwa jina la Yehova, akisema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, hutakuwa na hatia yoyote kuhusu jambo hili!”

11 Basi mwanamke huyo akamuuliza: “Nikupandishie nani?” Akajibu: “Nipandishie Samweli.”

12 Mwanamke huyo alipomwona “Samweli,”^{*c} akapiga kelele kwa sauti yake yote na kumwambia Sauli: “Kwa nini ulinidanganya? Wewe ni Sauli!”

13 Mfalme akamwambia: “Usiogope, lakini unaona nini?” Mwanamke huyo akamjibu Sauli: “Ninaona mtu fulani kama mungu akipanda kutoka duniani.”

14 Mara moja Sauli akamuuliza mwanamke huyo: “Yukoje?” akamwambia: “Ni mwanamu-me mzee anayepanda, amevaa joho lisilo na mikonu.”^d Ndipo Sauli akatambua kwamba ni “Samweli,” naye akainama chini kifudufudi na kusujudu.

15 Kisha “Samweli” akamuuliza Sauli: “Kwa nini umenibusua kwa kufanya nipandishwe?” Sauli akamjibu: “Niko katika taabu kubwa. Wafilisti wanapigana nami, na Mungu ameniacha, hanijibu tena, iwe ni kupitia manabii au katika ndoto;^e ndiyo sababu nimekuita uniambie ninilopaswa kufanya.”^f

16 “Samweli” akamuuliza: “Kwa nini unaniomba ushauri wakati ambapo Yehova amekuacha^g na kuwa adui yako?”

17 Yehova atajifanyia mwenyewe yale aliyotabiri kupitia mimi: Yehova ataurarua ufal-

SURA YA 28

a 1Sa 28:3

b Kut 22:18
Law 20:27

c 1Sa 28:3

d 1Sa 15:27

e 1Sa 28:6

f Law 19:31

g 1Sa 15:23
1Sa 16:14

Safu ya 2

a 1Sa 13:14
1Sa 15:28
1Sa 16:13
1Sa 24:20

b 1Sa 15:9
1Nya 10:13

c 1Sa 28:1
1Sa 31:1

d 1Sa 31:5

e 1Sa 31:2
2Sa 2:8

f 1Sa 31:7

g Law 20:27

me kutoka mikononi mwako na kumpa mwenzako, Daudi.^a

18 Kwa sababu hukuitii sauti ya Yehova, nawe hukutekeleza hasira yake kali dhidi ya Waa-maleki,^b ndiyo sababu Yehova anakutendea mambo haya leo.

19 Pia, Yehova atakutia wewe pamoja na Waisraeli mikononi mwa Wafilisti,^c na kesho wewe^d na wana wako^e mtakuwa pamoja nami. Yehova atalitia pia jeshi la Israeli mikononi mwa Wafilisti.”^f

20 Papo hapo Sauli akaanguka chini akiwa amenyooka mwili mzima naye akaogopa sana kwa sababu ya maneno ya “Samweli.” Nguvu zikamwishia, kwa sababu hakuwa amekula chakula mchana wote na usiku kucha.

21 Mwanamke huyo alipomkaribia Sauli na kuona kwamba ana wasiwasi mwingi, akamwambia: “Mimi kijakazi wako nimetii jambo ulilosema, na nimehatarisha uhai wangu^{*g} kwa kufanya ulioniambia nifanye.”

22 Sasa, tafadhali, sikiliza maneno ninayotaka kukwambia mimi mtumishi wako. Acha ni kuandalie kipande cha mkate, ule ili upate nguvu za kuen-delea na safari.”

23 Lakini akakataa na kusema: “Sitakula.” Hata hivyo, watumishi wake na pia mwanamke huyo wakaendelea kumsihi ale. Mwishowe akawasikiliza, akainuka kutoka ardhini na kuketi kitandani.

24 Mwanamke huyo alikuwa na ndama aliyenona nyumbani mwake, basi akamchinja* haraka, akachukua unga, akaukanda na kuoka mikate isiyu na chachu.

28:21 *Au “nimetia nafsi yangu mikononi mwangu.” **28:24** *Au “akamtoa dhahibu.”

28:12 *Au “mtu aliyonekana kama Samweli.”

25 Akamwandalia Sauli na watumishi wake, nao wakala. Kisha wakaondoka na kwenda zao usiku huo.^a

29 Wafilisti^b walikusanya majeshi yao yote kule Afeki Waisraeli walipokuwa wakipiga kambi karibu na chemchemi huko Yezreeli.^c **2** Na watawala wa Wafilisti walikuwa wakipita wakiwa na vikosi vyao vya mamia na maelfu, naye Daudi na wanaume wake walikuwa wakiwafuata nyuma wakiwa na Akishi.^d **3** Lakini wakuu wa Wafilisti wakauliza: “Waebrania hawa wamekuja kufanya nini?” Akishi akawajibu hivi wakuu wa Wafilisti: “Huyu ni Daudi, mtumishi wa Mfalme Sauli wa Israeli, naye ameshi pamoja nami kwa mwaka mmoja au zaidi.^e Tangu siku aliyokimbilia kwangu mpaka leo sijampata na kosa lolote.” **4** Lakini wakuu wa Wafilisti wakamkasirikia vikali Akishi na kumwambia: “Mrudishe mtu huyu.^f Acha arudi mahali ulipompa. Usimruhusu ashuke kwenda pamoja nasi vitani, asije akatugeuka na kutushambulia wakati wa vita.^g Kuna njia gani bora ya mtu huyu kupata kibali cha bwana wake isipokuwa kumpelekea vichwa vya wanaume wetu? **5** Je, huyu si Daudi waliyeimba kumhusu wali-pocheza dansi, wakisema:

‘Sauli ameua maelfu yake, Na Daudi makumi yake ya maelfu?’^h

6 Basi Akishiⁱ akamwita Daudi na kumwambia: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, wewe ni mnyoofu, nami ningependa uende vitani pa-

SURA YA 28
a 1Sa 28:8

SURA YA 29
b 1Sa 28:1

c Yos 19:17, 18
1Sa 29:11

d 1Sa 28:2

e 1Sa 27:7, 12

f 1Nya 12:19

g 1Sa 14:21

h 1Sa 18:7
1Sa 21:11

i 1Sa 21:10
1Sa 27:2

Safu ya 2
a 1Sa 28:2

b 1Sa 27:11, 12

c 1Sa 29:3, 9

d 1Sa 27:12

e Yos 19:17, 18
1Sa 29:1

SURA YA 30
f Yos 15:21, 31
1Sa 27:5, 6

g Mwa 36:12
Kut 17:14
1Sa 15:2
1Sa 27:8

h 1Sa 27:3

moja na jeshi langu,^a kwa sababu tangu siku uliyokuja kwangu mpaka leo sijakupata na kosa lolote.^b Lakini watawala hawakuamini.^c **7** Hivyo rudi kwa amani, na usifanye jambo lolote ambalo halitawapendeza watawala wa Wafilisti.” **8** Lakini Daudi akamuuliza Akishi: “Kwa nini? Nimefanya nini? Ni kosa gani ambalo umenipata nalo mimi mtumishi wako tangu siku niliyokuja kwako mpaka leo? Kwa nini nisiende pamoja nawe kupigana na maadui wako, bwana wangu mfalme?” **9** Akishi akamjibu hivi Daudi: “Kwa maoni yangu, umekuwa mwema kama malaika wa Mungu.^d Lakini wakuu wa Wafilisti wamesema, ‘Usimruhusu apande pamoja nasi kwenda vitani.’ **10** Sasa amka asubuhi na mapema pamoja na watumishi wa bwana wako walio-kuja nawe; amkeni na kuondoka asubuhi na mapema mara tu kutakapopambazuka.”

11 Basi Daudi na wanaume wake wakaamka asubuhi na mapema ili warudi katika nchi ya Wafilisti, nao Wafilisti wakapanda kwenda Yezreeli.^e

30 Daudi na wanaume wake walipofika Siklagi^f siku ya tatu, Waamaleki^g walikuwa wamevamia upande wa kusini* na pia Siklagi, nao walikuwa wameshambulia Siklagi na kuliteketeza kwa moto. **2** Walikuwa wamewateka wanawake^h na watu wote walio-kuwa humo, kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi. Hawakumuua yeyote, lakini waliwachukua na kwenda zao. **3** Daudi na wanaume

30:1 * Au “Negebu.”

wake walipofika jijini, waliku-
ta jiji lote limeteketewa, na
wake zao na wana wao na ma-
binti wao walikuwa wamechu-
kuliwa mateka. **4** Basi Dau-
di na wanaume waliokuwa pa-
moja naye wakaanza kulia kwa
sauti kubwa mpaka wakako-
sa nguvu za kuendelea kulia.
5 Wake wawili wa Daudi wa-
likuwa pia wametekwa, Ahi-
noamu wa Yezreeli na Abigai-
li mjane wa Nabali Mkarme-
li.^a **6** Daudi alifadhaika sana,
kwa sababu wanaume wake
walitaka kumpiga mawe, kwa
maana wanaume wote waliku-
wa na uchungu mwingi sana
kwa kuwapoteza wana na ma-
binti wao. Lakini Daudi akaji-
tia nguvu kwa msaada wa Ye-
hova Mungu wake.^b

7 Kisha Daudi akamwambia
kuhani Abiathari,^c mwana wa
Ahimeleki: “Tafadhali iletie ile
efodi hapa.”^d Kwa hiyo Abia-
thari akamletea Daudi hiyo
efodi. **8** Daudi akamuuliza
Yehova:^e “Je, nilifuatie kundi
hili la wavamizi? Je, nitawa-
fikia?” Ndipo Akamwambia:
“Wafuatie, kwa maana hakika
utawafikia, nawe utawaokoa
waliotekwa.”^f

9 Mara moja Daudi akaon-
doka na wanaume 600^g wa-
liokuwa pamoja naye, wa-
kaenda mpaka kwenye Ko-
rongo* la Besori, na wanaume
kadhaa wakabaki hapo.
10 Daudi akaendelea kuwa-
fuatia akiwa na wanaume 400,
lakini wanaume 200 walioku-
wa wamechoka sana wasiwe-
ze kuvuka Korongo la Besori
wakabaki hapo.^h

11 Wanaume hao wakamku-
ta mwanamume fulani Mmisiri

SURA YA 30

a 1Sa 25:42
1Sa 25:43

b Zb 18:6
Zb 31:1,9
Zb 34:19
Zb 143:5

c 1Sa 22:20
1Fa 2:26

d 1Sa 23:9

e Hes 27:21
Amu 20:28
1Sa 23:2,11
1Sa 28:6

f 1Sa 30:18
Zb 34:19

g 1Sa 23:13
1Sa 27:2

h 1Sa 30:21

Safu ya 2

a 2Sa 8:18
1Fa 1:38
1Nya 18:17
Eze 25:16
Sef 2:5

b Yos 14:13

c Kut 17:14

d 1Sa 30:3

mbugani na kumpeleka kwa
Daudi. Wakampa chakula na
maji ya kunywa, **12** na pia
kipande cha keki ya tini zili-
zoshinikizwa na keki mbili za
zabibu kavu. Baada ya kula,
akapata nguvu,* kwa saba-
bu hakuwa amekula chaku-
la chochote wala kunywa maji
kwa siku tatu, mchana na usi-
ku. **13** Sasa Daudi akamuuli-
za: “Wewe ni mtumishi wa
nani, na unatoka wapi?” aka-
jibu: “Mimi ni mtumishi Mmi-
sri, mtumwa wa Mwamaleki
fulani, lakini bwana wangu
aliniacha kwa sababu nilishi-
kwa na ugonjwa siku tatu zi-
lizopita. **14** Tulivamia upa-
nde wa kusini wa* Wakerethi^a
na eneo la Yuda na upande wa
kusini wa* Kalebu,^b nasi tu-
kateketeza Siklagi kwa moto.”
15 Daudi akamuuliza: “Je,
utaniongoza chini kwenye ku-
ndi hilo la wavamizi?” Akajibu:
“Ukiniapia mbele za Mungu
kwamba hutaniau wala kuni-
tia mikononi mwa bwana wan-
gu, nitakuongoza chini kwe-
nye kundi hilo la wavamizi.”

16 Basi akamwongoza chini
mahali walipokuwa wameenea
kotekote, wakila na kunywa
na kusherehekea kwa saba-
bu ya nyara nyingi sana wa-
lizokuwa wamechukua kuto-
ka katika nchi ya Wafilisti na
nchi ya Yuda. **17** Kisha Dau-
di akawaua kuanzia asubuhi
kabla ya mapambazuko mpa-
ka jioni siku iliyofuata; haku-
na mtu yeyote aliyeponyoka^c
isipokuwa wanaume 400 wa-
liopanda ngamia na kuki-
mbia. **18** Daudi akapata vitu
vyote ambavyo Waamaleki
walikuwa wamechukua,^d naye

30:12 *Tnn., “roho yake ikamrudia.”

30:14 *Au “Negebu ya.”

akawaokoa wake zake wawili. **19** Hawakukosa kitu chochote kilichokuwa chao, kuanzia kidogo zaidi mpaka kikubwa zaidi. Waliwapata wana mabinti wao na kuchukua nyara;^a Daudi alipata kila kitu walichochukua. **20** Basi Daudi akachukua makundi yote ya kondoo na ng'ombe, nao wawakatanguliza wanyama hao mbele ya mifugo yao wenyewe. Wakasema: "Hizi ni nyara za Daudi."

21 Kisha Daudi akafika kwa wale wanaume 200 waliobaki kwenye Korongo la Besorri^b kwa sababu waliukwa wamechoka sana wasiweze kwenenda naye, nao wakaja kumpokea Daudi na watu waliokuwa pamoja naye. Daudi alipofika karibu na wanaume hao, akawajulia hali. **22** Hata hivyo, kila mtu mbaya na asiyefaa kitu kati ya watu walioenda na Daudi akasema: "Kwa kuwa hawakwenda pamoja nasi, hatutawapa nyara yoyote tuliyo chukua, lakini kila mmoja wao anaweza kumchukua mke wake na wanawe na kwenenda zake." **23** Hata hivyo, Daudi akasema: "Msifanye hivyo ndugu zangu kuhusiana na vitu ambavyo Yehova ametupatia. Alitulinda na kulitia mikononi mwetu kundi la wavamizi lililokuja kutuvamia."^c **24** Ni nani atakayekubaliana nanyi katika jambo hili? Fungu la yule aliyeshuka kwenenda vitani litakuwa sawa na fungu la yule aliyeketi kando ya mizigo.^d Wote watapata fungu lilelile."^e **25** Na kuanzia siku hiyo na kuendelea, akalifanya jambo hilo kuwa sheria na amri katika Israeli mpaka leo hii.

SURA YA 30

a 1Sa 30:8
Zb 34:19

b 1Sa 30:10

c 1Sa 30:8

d 1Sa 30:10

e Hes 31:27
Yos 22:8
Zb 68:12

Safu ya 2

a Yos 19:4, 8

b Yos 15:20, 48
Yos 21:8, 14c Yos 15:20, 50
Yos 21:8, 14d 1Sa 27:10
1Nya 2:9e Amu 1:16
1Sa 15:6f Hes 21:3
Yos 19:1, 4
Amu 1:17g Yos 14:13
2Sa 2:1

SURA YA 31

h 1Sa 14:52
1Sa 29:1i 1Sa 28:4
2Sa 1:21
1Nya 10:1-5

j 1Sa 13:2

k 1Nya 8:33

l 2Sa 1:4, 6

m 1Sa 17:26
2Sa 1:20

26 Daudi aliporudi Siklagi, aliwapelekea wazee wa Yuda waliokuwa rafiki zake baadhi ya nyara hizo, akisema: "Hii ni zawadi* yenu kutoka katika nyara za maadui wa Yehova."^a **27** Alizipeleka kwa wale waliokuwa Betheli,^a kwa wale waliokuwa Ramothi la Negebu,^a kwa wale waliokuwa Yatiri,^b **28** kwa wale waliokuwa Aroeri, kwa wale waliokuwa Sifmothi, kwa wale waliokuwa Eshtemoa,^c **29** kwa wale waliokuwa Rakali, kwa wale waliokuwa katika majiji ya Wayerahmeeli,^d kwa wale waliokuwa katika majiji ya Wakeni,^e **30** kwa wale waliokuwa Horma,^f kwa wale waliokuwa Borashani, kwa wale waliokuwa Athaki, **31** kwa wale waliokuwa Hebroni,^g na sehemu zote ambazo Daudi na wanaume wake walitembelea kwa ukawaida.

31 Sasa Wafilisti walikuwa wakipigana na Waisraeli.^h Na wanaume wa Israeli wakawakimbia Wafilisti, na wengi wakauawa kwenye Mlima Gilboa.ⁱ **2** Wafilisti wakamkaribia sana Sauli na wanawe, nao wakamuua Yonathani,^j Abinadabu, na Malki-shua, wana wa Sauli.^k **3** Vita vikawa vikali sana dhidi ya Sauli, na wapiga mishale wakampata na kumjehuruhi vibaya.^l **4** Ndiope Sauli akamwambia mtu aliyembebea silaha: "Chomoa upanga wako unichome nao, ili watu hawa wasiotahiriwa^m wasije kuni-choma kwa upanga na kunitendea kikatili."ⁿ Lakini mtu huyo aliyembebea silaha hakutaka kufanya hivyo, kwa sa-

30:26 *Tnn., "baraka." 30:27 *Tnn., "la kusini." 31:4 *Au "na kunitesa."

babu aliogopa sana. Basi Sauli akachukua upanga na kuuangukia.^a **5** Mtu aliyembebea silaha alipoona kwamba Sauli amekufa,^b yeye pia akauangukia upanga wake mwenyewe, akafa pamoja naye. **6** Basi Sauli, wanawe watatu, mtu aliyembebea silaha, na wanau-me wake wote wakafa pamoja siku hiyo.^c **7** Watu wa Israeli waliokuwa katika eneo la bondeni na katika eneo la Yordani walipoona kwamba wanau-me wa Israeli wamekimbia na kwamba Sauli na wanawe wamekufa, wakaanza kuyaacha majiji na kukimbia;^d kisha Wafilisti wakaja na kukaa humo.

8 Siku iliyofuata, Wafilisti walipokuja kuwavua walioua-wa vitu walivyokuwa navyo, walimkuta Sauli na wanawe watatu wakiwa wameanguka kwenye Mlima Gilboa.^e **9** Basi wakamkata kichwa na

SURA YA 31

a 1Nya 10:4

b 1Sa 26:10
1Nya 10:13c 1Sa 28:19
1Nya 10:6,7

d 1Sa 13:6

e 1Sa 28:4
1Sa 31:1
2Sa 1:6
1Nya 10:8-12

Safu ya 2

a 2Sa 1:20

b Amu 16:23

c Yos 17:11
Amu 1:27

d 1Sa 11:1,9-11

e 2Sa 21:12

f 2Sa 2:4,5

kumvua silaha zake na kutuma ujumbe kotekote katika nchi ya Wafilisti ili habari^a zienezwe katika nyumba za* sanamu zao^b na miongoni mwa watu. **10** Kisha waka-weka silaha zake katika nyumba ya sanamu za Ashtorethi na kuitundika maiti yake kwenye ukuta wa Beth-shani.^c **11** Wakaaji wa Yabeshi-gileadi^d waliposikia mambo ambayo Wafilisti walikuwa wamemtendea Sauli, **12** mashujaa wote wakaondoka na kusafiri usiku kucha, wakaondoa maiti za Sauli na wanawe kutoka kwenye ukuta wa Beth-shani. Wakarudi Yabeshi na kuzichoma moto huko. **13** Kisha wakachukua mifupa yao^e na kuizika chini ya mti wa mwesheli huko Yabeshi,^f nao wakafunga kwa siku saba.

31:9 *Au "mahekalu ya."

KITABU CHA PILI CHA

SAMWELI

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Daudi apata habari za kifo cha Sauli (1-16)
Daudi aimba wimbo wa kumwombolezea Sauli na Yonathani (17-27)</p> <p>2 Daudi, mfalme wa Yuda (1-7)
Ish-boshethi, mfalme wa Israeli (8-11)
Vita kati ya nyumba ya Daudi na nyumba ya Sauli (12-32)</p> <p>3 Nyumba ya Daudi yazidi kupata nguvu (1)
Wana wa Daudi (2-5)
Abneri ajiunga na Daudi (6-21)</p> | <p>Yoabu amua Abneri (22-30)
Daudi amwombolezea Abneri (31-39)</p> <p>4 Ish-boshethi auawa (1-8)
Daudi aagiza waliomuua Ish-boshethi wauawe (9-12)</p> <p>5 Daudi awekwa kuwa mfalme wa nchi yote ya Israeli (1-5)
Yerusalemu latekwa (6-16)
Sayuni, Jiji la Daudi (7)
Daudi awashinda Wafilisti (17-25)</p> <p>6 Sanduku la agano laletwa Yerusalemu (1-23)</p> |
|--|--|

- Uza alikamata sanduku la agano na kuuawa (6-8)
Mikali amdharau Daudi (16, 20-23)
- 7 Daudi hatajenga hekalu (1-7)
Agano pamoja na Daudi kwa ajili ya ufalme (8-17)
Sala ya Daudi ya shukrani (18-29)
- 8 Ushindi mbalimbali wa Daudi (1-14)
Wakuu katika utawala wa Daudi (15-18)
- 9 Daudi amtendea Mefiboshethi kwa upendo mshikamanifu (1-13)
- 10 Awashinda Waamoni na Wasiria (1-19)
- 11 Daudi afanya uzinzi na Bath-sheba (1-13)
Daudi apanga Uria auawe (14-25)
Daudi amchukua Bath-sheba kuwa mke wake (26, 27)
- 12 Nathani amkaripia Daudi (1-15a)
Mwana wa Bath-sheba afa (15b-23)
Bath-sheba amzaa Sulemani (24, 25)
Jiji la Raba la Waamoni latekwa (26-31)
- 13 Amnoni ambaka Tamari (1-22)
Absalomu amua Amnoni (23-33)
Absalomu akimbilia Geshuri (34-39)
- 14 Yoabu na mwanamke Mtekoa (1-17)
Daudi agundua njama ya Yoabu (18-20)
Absalomu aruhusiwa kurudi (21-33)
- 15 Njama na uasi wa Absalomu (1-12)
Daudi akimbia kutoka Yerusalemu (13-30)
Ahithofeli ajiunga na Absalomu (31)
Hushai atumwa kuvuruga ushauri wa Ahithofeli (32-37)
- 16 Siba amchongea Mefiboshethi (1-4)
Shimei amtukana Daudi (5-14)
Absalomu ampokea Hushai (15-19)
Ushauri wa Ahithofeli (20-23)
- 17 Hushai avuruga ushauri wa Ahithofeli (1-14)
- Daudi aonywa; amtoroka Absalomu (15-29)
Barzilai na wengine wamletea vyakula (27-29)
- 18 Absalomu ashindwa; kifo chake (1-18)
Daudi ajulishwa kuhusu kifo cha Absalomu (19-33)
- 19 Daudi amwombolezea Absalomu (1-4)
Yoabu amkaripia Daudi (5-8a)
Daudi arudi Yerusalemu (8b-15)
Shimei aomba msamaha (16-23)
Mefiboshethi athibitishwa kuwa hana hatia (24-30)
Barzilai aheshimiwa (31-40)
Makabila yazozana (41-43)
- 20 Uasi wa Sheba; Yoabu amua Amasa (1-13)
Sheba afuatwa na kukatwa kichwa (14-22)
Wakuu katika utawala wa Daudi (23-26)
- 21 Nyumba ya Sauli yalipizwa kisasi kwa ajili ya Wagibeoni (1-14)
Vita dhidi ya Wafilisti (15-22)
- 22 Daudi amsifu Mungu kwa sababu ya matendo yake ya wokovu (1-51)
“Yehova ni jabali langu” (2)
Yehova ni mshikamanifu kwa walio washikamanifu (26)
- 23 Maneno ya mwisho ya Daudi (1-7)
Mambo yaliyotendwa na mashujaa hodari wa Daudi (8-39)
- 24 Dhambi ya Daudi ya kuwahesabu watu (1-14)
Ugonjwa hatari wasababisha vifo vya watu 70,000 (15-17)
Daudi ajenga madhabahu (18-25)
Hatatoa dhabihu ambazo hazimgharimu (24)

1 Baada ya kifo cha Sauli, Daudi aliporudi baada ya kuwashinda* Waamaleki, alika Siklagi^a kwa siku mbili.
2 Siku ya tatu, mtu fulani alikuja kutoka katika kambi ya

SURA YA 1

^a 1Sa 27:5, 6

Sauli akiwa amevaa nguo zilizozoruka, na akiwa na mavumbi kichwani. Alipomkaribia Daudi, alijianguka chini na kumwinamia.

3 Daudi akamuuliza: “Umetoka wapi?” Akajibu: “Nimetoroka katika kambi ya Israeli.”

1:1 *Au “kuwaua.”

4 Daudi akamuuliza: “Ni nini kilichotokea? Tafadhali niambie.” Akamwambia: “Watu wamekimbia kutoka vitani na wengi wameanguka na kufa. Hata Sauli na Yonathani mwanawe wamekufa.”^a **5** Kisha Daudi akamuuliza hivi kijana huyo aliyemletea habari: “Unajuaje kwamba Sauli na Yonathani mwanawe wamekufa?” **6** Kijana huyo akajibu: “Nilifika kwenye Mlima Gilboa^b bila kutazamia, nika mwona Sauli akiwa ameegemea mkuki wake, na magari ya vita na wapanda farasi walikuwa wamemfikia.”^c **7** Ali-pogeuka na kuniona, aliniita, nami nikasema, ‘Naam!’ **8** Akaniuliza, ‘Wewe ni nani?’ nikajibu, ‘Mimi ni Mwamaleki.’^d **9** Kisha akasema, ‘Tafadhali, nikaribie unie, kwa maana nina maumivu makali sana, lakini bado niko hai.’ **10** Basi nikamkaribia na kumuua,^e kwa maana nilijua kwamba hangeendelea kuishi baada ya kuanguka chini akiwa amejeruhiwa. Kisha nikachukua taji lililokuwa kichwani mwake na kikuku kilichokuwa mkononi mwake, nami nimevileta hapa kwako bwana wangu.”

11 Ndipo Daudi akashika mavazi yake na kuyararua, na watu wote waliokuwa pamoja naye wakafanya vivyo hivyo. **12** Nao wakaomboleza na kulia na kufunga^f mpaka jioni kwa ajili ya Sauli, kwa ajili ya Yonathani mwanawe, kwa ajili ya watu wa Yehova, kwa ajili ya nyumba ya Israeli,^g kwa sababu walikuwa wameuawa kwa upanga.

13 Daudi akamuuliza hivi kijana aliyemletea habari:

SURA YA 1

a 1Sa 31:1, 6
1Nya 10:4, 6

b 1Sa 28:4
1Nya 10:1

c 1Sa 31:3
1Nya 10:3

d Kut 17:16
Kum 25:19
1Sa 15:20
1Sa 30:1

e 1Sa 31:4

f 1Sa 31:11, 13

g 1Sa 31:1

Safu ya 2

a Hes 12:8
1Sa 24:6
1Sa 26:9
1Sa 31:4

b 2Sa 4:10

c 2Sa 1:6, 10

d 1Sa 31:6

e Yos 10:13

f 1Sa 31:8

g 1Sa 31:9

h 1Sa 31:1
1Nya 10:1

i Law 27:16

“Unatoka wapi?” Akajibu: “Mimi ni mwana wa mkaaaji mgeni, Mwamaleki.” **14** Kisha Daudi akamuuliza: “Kwa nini hukuogopa kuinua mkonono wako kumuua mtiwamafuta wa Yehova?”^a **15** Ndipo Daudi akamwita kijana mmoja na kumwambia: “Njoo umuue.” Basi akampiga na kumuua.^b **16** Daudi akamwambia: “Damu yako na iwe juu ya kichwa chako mwenyewe, kwa sababu kinywa chako mwenyewe kilitoa ushahidi dhidi yako, uliposema, ‘Mimi mwenyewe nilimuua mtiwamafuta wa Yehova.’”^c

17 Kisha Daudi akaimba wimbo huu wa maombolezo kwa ajili ya Sauli na Yonathani mwanawe^d **18** na kusema kwamba watu wa Yuda wafundishwe wimbo wa maombolezo unaoitwa “Upinde,” ulioandikwa katika kitabu cha Yashari:^e

19 “Ee Israeli, uzuri umeuawa kwenye vilima vyako.^f

Jinsi walivyoanguka wanaume wenye nguvu!

20 Msiseme jambo hilo kule Gathi,^g

Msilitagaze katika barabara za Ashkeloni,

Mabinti wa Wafilisti wasije wakashangilia,

Mabinti wa watu wasio-tahiriwa wasije wakafurahi.

21 Enyi milima ya Gilboa,^h Msipate umande wowote wala mvua yoyote, Wala mashamba yanayozaa michango mitakatifu,ⁱ

Kwa sababu ngao ya wenye nguvu ilichafuliwa huko, Sasa ngao ya Sauli haijatiwa mafuta.

- 22** Kutoka kwenye damu ya waliouawa, kutoka kwenye mafuta ya wenye nguvu,

Upinde wa Yonathani haukurudi nyuma,^a

Na upanga wa Sauli haukurudi bila mafanikio.^b

- 23** Sauli na Yonathani,^c watu waliopondwa na kuthaminiwa* walipokuwa hai, Na katika kifo hawakute-nganishwa.^d

Walikuwa wepesi kuliko tai,^e

Walikuwa wenye nguvu kuliko simba.^f

- 24** Enyi mabinti wa Israeli, mlilieni Sauli, Aliyewavisha nguo nyekundu na mapambo, Aliyelia mapambo ya dhababu kwenye nguo zenu.

- 25** Jinsi wenye nguvu wali- vyoanguka vitani! Yonathani amelala akiwa ameuawa juu ya vilima vyenu!^g

- 26** Nimehuzunika kwa ajili yako, ndugu yangu Yonathani;

Nilikupenda sana.^h

Upendo wako kwangu ulikuwa mzuri sana kuliko upendo wa wanawake.ⁱ

- 27** Jinsi wenye nguvu wali- vyoanguka Na silaha za vita kuangamia!"

2 Baadaye Daudi akamuuli- za hivi Yehova: "Je, nipande kwenda katika mojawapo ya majiji ya Yuda?" Yehova

1:23 *Au "kupendeza."

SURA YA 1

a 1Sa 18:4

1Sa 20:20

b 1Sa 14:47

c 1Sa 18:1

d 1Sa 31:6

1Nya 10:6

e Ayu 9:26

f Met 30:30

g 1Sa 31:8

h 1Sa 18:1, 3

i 1Sa 19:2

1Sa 20:17, 41

1Sa 23:16-18

Met 17:17

Met 18:24

SURA YA 2

j Hes 27:21

1Sa 28:6

Safu ya 2

a Mwa 23:2

Hes 13:22

Yos 14:14

Yos 20:7

2Sa 5:1

1Fa 2:11

b 1Sa 25:43

c 1Sa 25:42

1Sa 30:5

d 1Sa 22:1, 2

1Sa 27:2

1Nya 12:1

e Mwa 49:10

1Sa 15:24, 28

1Sa 16:13

2Sa 5:4, 5

1Nya 11:3

f 1Sa 31:11-13

g 2Sa 9:7

2Sa 10:2

h 1Sa 14:50

1Sa 17:55

1Sa 26:5

2Sa 4:1

1Fa 2:5

i 2Sa 4:5-8

2Sa 4:12

j Mwa 32:1, 2

Yos 13:29, 30

k Yos 13:8, 11

l Yos 19:17, 18

m Yos 16:5-8

akamwambia: "Panda uende." Kisha Daudi akamuuliza: "Ninde wapi?" Akajibu: "Hebroni."^a **2** Basi Daudi akapanda kwenda huko na wake zake wawili, Ahinoamu^b wa Yezreeli na Abigaili^c mjane wa Nabali Mkarmeli. **3** Daudi akawachukua pia wanaume walio- kuwa pamoja naye,^d kila mmoja na familia yake, nao wakakaa katika majiji yanayozunguka Hebroni. **4** Kisha wanaume wa Yuda wakaja, na huko wakamtia mafuta Daudi awe mfalme juu ya nyumba ya Yuda.^e

Wakamwambia Daudi: "Watu wa Yabesh-gileadi ndio waliomzika Sauli." **5** Basi Daudi akawatuma wajumbe kwa watu wa Yabesh-gileadi na kuwaambia: "Yehova na awabari- ki, kwa sababu mlimtendea bwana wenu, Sauli, kwa upendo mshikamanifu kwa kumzika.^f **6** Yehova na awatendee kwa upendo mshikamanifu na uaminifu. Mimi pia nitawatendea fadhili kwa sababu mme- fanya jambo hili.^g **7** Sasa mikono yenu na iwe na nguvu, nanyi muwe jasiri kwa saba- bu bwana wenu Sauli ameku- fa, na nyumba ya Yuda imenitia mafuta niwe mfalme juu yao."

8 Lakini Abneri^h mwana wa Neri mkuu wa jeshi la Sauli, alikuwa amemchukua Ish- boshethi,ⁱ mwana wa Sauli, akamvusha mpaka Mahanaimu/ **9** na kumfanya kuwa mfalme wa Gileadi,^k wa Waa- shuri, Yezreeli,^l Efraimu,^m Ben- jamini, na juu ya Waisraeli wote. **10** Ish-boshethi, mwana wa Sauli, alikuwa na umri wa miaka 40 alipokuwa mfal- me wa Israeli, naye alitawa-

la kwa miaka miwili. Hata hivyo, nyumba ya Yuda ilimuunga mkono Daudi.^a **11** Muda ambao Daudi alikuwa mfalme huko Hebroni juu ya nyumba ya Yuda ulikuwa miaka saba na miezi sita.^b

12 Baada ya muda Abneri mwana wa Neri na watumishi wa Ish-boshethi, mwana wa Sauli, wakatoka Mahanaimu^c na kwenda Gibeoni.^d **13** Yoabu^e mwana wa Seruya^f na watumishi wa Daudi wakaondoka pia na kukutana nao kwenye kidimbwi cha Gibeoni; kikundi kimoja kiliketi upande mmoja wa kidimbwi hicho na kikundi cha pili upande wa pili. **14** Hatimaye Abneri akamwambia hivi Yoabu: "Acha vijana wasimame na kupambana* mbele yetu." Ndipo Yoabu akasema: "Acha wasimame." **15** Basi wakasimama, wakahesabiwa na kuvuka, 12 wa Benjamini na Ish-boshethi mwana wa Sauli, na 12 kutoka kati ya watumishi wa Daudi. **16** Kila mmoja alimkamata mwenzake kichwani na kumchoma kwa upanga ubavuni, na wote wakaanguka pamoja. Basi mahali hapo huko Gibeoni pakaitwa Helkath-hasurimu.

17 Vita vikawa vikali sana siku hiyo, mwishowe Abneri na wanaume wa Israeli wakashindwa na watumishi wa Daudi. **18** Basi wana watautu wa Seruya^g walikuwa mahali hapo—Yoabu,^h Abishai,ⁱ na Asaheli;^j naye Asaheli alikuwa na mbio sana* kama swala katika nchi tambarare. **19** Asaheli akamkimbi-

2:14 *Au "kushindana." 2:18 *Tnn., "alikuwa na miguu myepesi."

SURA YA 2

a 2Sa 2:4

b 1Nya 3:4

c 2Sa 2:8

d Yos 10:12
Yos 18:21, 25
Yos 21:8, 17
2Sa 20:8
2Nya 1:3e 2Sa 8:16
2Sa 20:23
1Fa 1:5, 7

f 1Nya 2:15, 16

g 1Nya 2:15, 16

h 2Sa 10:7
2Sa 24:2
1Fa 11:15
1Nya 11:6i 1Sa 26:6
2Sa 20:6
1Nya 11:20j 2Sa 3:27
2Sa 23:24
1Nya 27:1, 7

Safu ya 2

a 2Sa 3:27

za Abneri, naye hakugeuka kulia wala kushoto alipokuwa akimkimbiza. **20** Abneri alipotazama nyuma, aliuliza: "Ni wewe Asaheli?" akajibu: "Naam, ni mimi." **21** Ndipo Abneri akamwambia: "Nenda kulia au kushoto umkamate kijana mmoja na kuchukua vitu vyake." Lakini Asaheli hakutaka kuacha kumkimbiza. **22** Basi Abneri akamwambia tena Asaheli: "Acha kunikimbiza. Kwa nini nikuue? Nitawezaje kumtazama usoni ndugu yako Yoabu?" **23** Lakini hakuacha kumkimbiza, basi Abneri akamchoma tumboni kwa ncha ya nyuma ya mkuki,^a na mkuki huo ukatokea mgongoni mwake; akaanguka na kufa papo hapo. Kila mtu aliyefika mahali ambapo Asaheli alianguka na kufa alisimama hapo kwa muda.

24 Kisha Yoabu na Abishai wakaenda kumfuatia Abneri. Jua lilipokuwa likitua, wakafika kwenye kilima cha Ama, kilicho ng'ambo ya Gia kwenye njia inayoelekea katika nyika ya Gibeoni. **25** Na Wabenjamini wakakusanyika na kumfuata Abneri, wakawa kundi moja, nao wakajiimarisha juu ya kilima fulani. **26** Kisha Abneri akamwita Yoabu na kumuuliza: "Je, upanga utaeendelea kuangamiza* bila kukoma? Je, hujui kwamba mwisho utakuwa mchungu tu? Basi, utangoja kwa muda gani ndipo uwaambie watu wache kuwafuatia ndugu zao?" **27** Yoabu akamwambia: "Kwa hakika kama Mungu wa kweli anavyoishi, usingesema, watu hawa wangeendelea

2:26 *Tnn., "kunyafua."

kuwafuatia ndugu zao mpa-
ka asubuhi.” **28** Sasa Yoabu
akapiga pembe, wanaume
wake wakaacha kuwafuatia
Waisraeli, na vita vikakoma.

29 Kisha Abneri na watu
wake wakapiga mwendo kupi-
tulia Araba^a usiku huo wote,
wakavuka Yordani na kupi-
ga mwendo kupitia katika bon-
de lote* na mwishowe waka-
fika Mahanaimu.^b **30** Baada
ya Yoabu kuacha kumfuatia
Abneri, akawakusanya watu
wote pamoja. Watumishi 19
wa Daudi walikosekana kuti-
a ndani Asaheli. **31** Lakini
watumishi wa Daudi waliku-
wa wamewashinda Wabenja-
mini na wanaume wa Abneri,
na wanaume 360 kati yao wa-
likuwa wameuawa. **32** Waka-
mchukua Asaheli^c na kumzika
katika kaburi la baba yake
huko Bethlehem.^d Kisha Yoabu
na wanaume wake wakapiga
mwendo usiku kucha, waka-
fika Hebroni^e wakati wa ma-
pambazuko.

3 Vita kati ya nyumba ya
Sauli na nyumba ya Daudi
viliendelea kwa muda mrefu;
Daudi akazidi kupata nguvu,^f
lakini nyumba ya Sauli ikazidi
kudhoofika hatua kwa hatua.^g

2 Wakati huo, Daudi akazaa
wana huko Hebroni.^h Mzaliwa
wake wa kwanza aliitwa
Amnoniⁱ na mama yake ali-
kuwa Ahinoamu^j wa Yezreeli.
3 Mzaliwa wake wa pili aliku-
wa Kileabu na mama yake ali-
kuwa Abigaili,^k mjane wa Na-
bali Mkarmeli; na wa tatu ali-
kuwa Absalomu^l mwana wa
Maaka, binti ya Talmalim^m mfal-
me wa Geshuri. **4** Wa nne

2:29 *Au labda, “kupitia eneo lote la
Bithroni.”

SURA YA 2

a Kum 1:7
Yos 12:2,3

b Yos 21:8,38
2Sa 2:8

c 2Sa 2:18
1Nya 2:15,16

d Mwa 35:19
Ru 4:11
1Sa 16:1

e 2Sa 2:1,3
1Nya 11:1

SURA YA 3

f 1Sa 15:27,28
1Sa 24:17,20
1Sa 26:25

g 2Sa 2:17

h 1Nya 3:1-4

i 2Sa 13:1

j 1Sa 25:43

k 1Sa 25:42

l 2Sa 15:12

m 2Sa 13:37

Safu ya 2

a 1Fa 1:5

b 2Sa 2:8

c 2Sa 21:8-11

d 2Sa 2:10

e 2Sa 16:21
1Fa 2:22

f 1Sa 15:27,28
Zb 78:70
Zb 89:20

g Amu 20:1
2Sa 24:2

h 2Sa 3:39

alikuwa Adoniya^a mwana wa
Hagithi, na wa tano alikuwa
Shefatia mwana wa Abitali.
5 Wa sita alikuwa Ithreamu
mwana wa Eglal, mke wa Dau-
di. Hao ndio wana ambao Dau-
di aliwazaa huko Hebroni.

6 Vita kati ya nyumba ya
Sauli na nyumba ya Daudi vi-
lipokuwa vikiendelea, Abne-
ri^b aliendelea kuimarisha cheo
chake katika nyumba ya Sau-
li. **7** Awali Sauli alikuwa na
suria aliyemitwa Rispa,^c binti
ya Aya. Baadaye Ish-boshethi^d
akamuuliza Abneri: “Kwa nini
ulifanya ngono na suria
wa baba yangu?”^e **8** Abneri
akakasirika sana kwa saba-
bu ya maneno ya Ish-boshethi
na kusema: “Je, mimi ni ki-
chwa cha mbwa kutoka Yuda?
Mpaka leo, nimeitendea kwa
upendo mshikamanifu nyu-
mba ya Sauli baba yako, ndu-
gu zake, na rafiki zake, nami
sijakusaliti kwa kukutia mi-
kononi mwa Daudi; lakini leo
unanishutumu kwa sababu ya
kosa linalohusu mwanamke.
9 Mungu na aniadhibu mimi
Abneri, tena vikali, nisipo-
mtendea Daudi kama Yeho-
va alivyomwapia:^f **10** kwa-
mba atauhambisha ufalme ku-
toka katika nyumba ya Sauli
na kuimarisha kiti cha ufal-
me cha Daudi juu ya Israeli
na juu ya Yuda, kuanzia Dani
mpaka Beer-sheba.”^g **11** Ish-
boshethi hakuthubutu ku-
mwambia Abneri hata neno
moja zaidi, kwa sababu ali-
mwogopa Abneri.^h

12 Papo hapo Abneri aka-
watuma wajumbe kwa Daudi,
akisema: “Nchi hii ni ya nani?”
Akaongezea: “Fanya agano
pamoja nami, nami nitafanya

lolote niwezalo* kuwageuza Waisraeli wote wawe upande wako.”^a **13** Daudi akamwambia: “Vema! Nitafanya agano pamoja nawe. Lakini nakuomba ufanye jambo moja tu, usithubutu kuja mbele yangu mpaka umlete kwanza Mikali,^b binti ya Sauli, utakapokuja kuniona.” **14** Kisha Daudi akawatuma wajumbe kwa Ish-boshethi,^c mwana wa Sauli, akisema: “Nipe mke wangu Mikali, niliyemchumbia kwa magovi 100 ya Wafilisti.”^d **15** Kwa hiyo Ish-boshethi akawatuma watu wamchukue Mikali kutoka kwa Paltieli^e mume, mwana wa Laishi. **16** Lakini mume wake akaenda pamoja naye, akamfua ta akilia mpaka Bahurimu.^f Kisha Abneri akamwambia: “Nenda zako, rudi!” Kwa hiyo akarudi.

17 Basi Abneri akatuma ujumbe kwa wazee wa Israeli, akisema: “Kwa muda fulani mlitaka Daudi awe mfalme wenu. **18** Sasa chukue ni hatua, kwa maana Yehova alimwambia hivi Daudi: ‘Kwa mkono wako wewe Daudi mtumishi wangu^g nitawaokoa watu wangu Waisraeli kutoka mikononi mwa Wafilisti na kutoka mikononi mwa maadui wao wote.’” **19** Ndipo Abneri akazungumza na watu wa Benjamini.^h Pia, Abneri akaenda kuzungumza na Daudi faraghani kule Hebroni ili kumwambia mambo ambayo Waisraeli na nyumba yote ya Benjamini walikuwa wamekubaliana.

20 Abneri alipofika kwa Daudi kule Hebroni akiwa na

3:12 *Tnn., “na tazama! mkono wangu uko pamoja nawe ili.”

SURA YA 3

a 2Sa 5:3

b 1Sa 18:20
1Sa 19:11
1Nya 15:29

c 2Sa 2:10

d 1Sa 18:25, 27

e 1Sa 25:44

f 2Sa 16:5
1Fa 2:8g 1Sa 13:14
1Sa 15:27, 28
1Sa 16:1, 13
Zb 89:3, 20
Zb 132:17
Mdo 13:22h 1Sa 10:20, 21
1Nya 12:29

Safu ya 2

a 2Sa 8:16

b 1Sa 14:50
2Sa 2:8, 22

c 1Sa 14:51

d 2Sa 3:20

wanaume 20, Daudi alimwandalia karamu pamoja na wanaume waliokuwa naye. **21** Halafu Abneri akamwambia Daudi: “Acha niende nikawakusanye pamoja Waisraeli wote kwako bwana wangu mfalme, ili wafanye agano pamoja nawe, nawe utakuwa mfalme juu ya kila kitu upendacho.”* Basi Daudi akamruhusu Abneri aende, akaenda zake kwa amani.

22 Wakati huohuo, watumishi wa Daudi na pia Yoabu walirudi baada ya kufanya uvamizi, walileta nyara nyingi sana. Abneri hakuwa tena pamoja na Daudi huko Hebroni, kwa maana alikuwa amemruhusu aende zake kwa amani. **23** Yoabu^a alipowasili na jeshi lote lililokuwa pamoja naye, aliambiwa hivi: “Abneri^b mwana wa Neri^c alikuja kwa mfalme, naye akamruhusu aende zake, na Abneri akaenda zake kwa amani.” **24** Basi Yoabu akaingia kwa mfalme na kumwambia: “Umefanya nini? Abneri alikuja kwako. Kwa nini ulimruhusu aende zake, akafanikiwa kutoroka? **25** Unamjua Abneri mwana wa Neri! Alikuwa hapa kukupumbaza, kuchunguza shughuli zako zote, na kujua kila jambo unalofanya.”

26 Basi Yoabu akaondoka mbele ya Daudi, akawatuma wajumbe wamfuatie Abneri, wakamkuta kwenye tanga la maji la Sira na kumrudisha; lakini Daudi hakujua lolote kuhusu jambo hilo. **27** Abneri aliporudi Hebroni,^d Yoabu akampeleka pembeni ndani ya lango ili

3:21 *Au “ambacho nafsi yako inatamani.”

azungumze naye faraghani. Hata hivyo, Yoabu akamchoma kwa upanga tumboni, naye akafa;^a kwa sababu alimuua* Asaheli ndugu yake.^b

28 Daudi aliposikia habari hizo baadaye, alisema: "Mimi na ufalme wangu hatuna hatia milele mbele za Yehova kwa sababu ya damu^c ya Abneri mwana wa Neri. **29** Na irudi juu ya kichwa cha Yoabu^d na juu ya nyumba yote ya baba yake. Nyumba ya Yoabu isikose kamwe mwanamume anayetokwa na umajimaji^e au mtu mwenye ukoma^f au mwanamume anayetumikia kwenye gurudumu la mfumaji* au anayeuawa kwa upanga au asiye na chakula!"^g **30** Basi Yoabu na Abishai^h ndugu yake wali-muua Abneriⁱ kwa sababu alimuua Asaheli ndugu yao vitani^j kule Gibeoni.

31 Kisha Daudi akamwambia Yoabu na watu wote waliokuwa pamoja naye: "Rarueni mavazi yenu na mvae nguo za magunia, mwombolezeeni Abneri kwa sauti." Mfalme Daudi mwenyewe alikuwa akitembea nyuma ya machelela ya kubebea maiti. **32** Walimzika Abneri huko Hebroni; na mfalme akalia kwa sauti kubwa kwenye kaburi la Abneri, na watu wote wakalia. **33** Mfalme akamwambia Abneri wimbo wa maombolezo akisema:

"Je, Abneri alipaswa kufa kama anavyokufa mtu mpumbavu?

34 Mikono yako haikuwa imefungwa,

3:27 *Tnn., "kwa sababu ya damu ya."

3:29 *Huenda maneno hayo yanarejelea mwanamume mlemavu aliyelazimika kufanya kazi ya wanawake.

SURA YA 3

a 1Fa 2:5

b 2Sa 2:22, 23

c Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:33
Kum 21:9

d Zb 7:16
Zb 55:23
Met 5:22

e Law 15:2

f Law 13:44
Hes 5:2

g Kum 27:24
Zb 109:2, 10

h 2Sa 2:24

i 2Sa 2:8

j 2Sa 2:23

Safu ya 2

a 1Fa 2:31, 32

b Amu 20:26

c 2Sa 3:28
1Fa 2:5

d 1Sa 14:50
2Sa 2:8
2Sa 3:12

e 2Sa 2:4

f 1Nya 2:15, 16

g 2Sa 19:13
2Sa 20:10

h 2Sa 3:29
1Fa 2:5, 34

SURA YA 4

i 2Sa 2:8

j 2Sa 3:27

Na miguu yako haikuwa imefungwa pingu.*

Ulianguka kama mtu anayeangushwa na wahalifu."^{#a}

Ndipo watu wote wakamli-lia tena.

35 Baadaye watu wote wakaja kumpa Daudi mkate wa faraja* kungali mchana, lakini Daudi akaapa hivi: "Mungu na aniadhibu, tena vikali, ikiwa nitaonja mkate au kitu kingine chochote kabla ya jua kutua!"^b **36** Watu wote wakaona jambo hilo, nalo likawapendeza. Watu wote walipendeza na jambo hilo kama walivyopendeza na mambo yote yaliyofanywa na mfalme.

37 Basi watu wote* na Waisraeli wote wakajua siku hiyo kwamba si mfalme aliyeagiza Abneri mwana wa Neri auawe.^c **38** Kisha mfalme akawaambia hivi watumishi wake: "Je, hamjui kwamba mkuu na mtu mashuhuri ameanguka leo katika Israeli?"^d **39** Niko dhaifu leo, ingawa nimetiwa mafuta kuwa mfalme,^e na wanaume hawa, wana wa Seruya,^f ni wakatili sana kwangu.^g Yehova na amlipe mtenda maovu kulingana na uovu wake mwenyewe."^h

4 Ish-boshethiⁱ mwana wa Sauli aliposikia kwamba Abneri amekufa huko Hebroni,^j alipoteza ujasiri* na Waisraeli wote wakashikwa na wasiwasi. **2** Kulikuwa na wanaume wawili waliosimamia makundi ya wavami-

3:34 *Tnn., "kwa shaba." #Tnn., "wana wa ukosefu wa uadilifu." 3:35 *Au "mkate wa maombolezo." 3:37 *Yaani, watu wote wa Daudi. 4:1 *Tnn., "miko-no yake ikalegea."

zi ya mwana wa Sauli: mmoja wao alitwa Baana na mwingine alitwa Rekabu. Walikuwa wana wa Rimoni Mbeerothi, wa kabila la Benjamini. (Kwa maana awali Beerothi^a pia lilihesabiwa kuwa sehemu ya Benjamini. **3** Wabeerothi walikimbilia Gitaimu,^b nao wamekuwa wakaaji wageni katika eneo hilo mpaka leo.)

4 Sasa Yonathani^c mwana wa Sauli alikuwa na mwana aliyelemaa miguu.^{*d} Alikuwa na umri wa miaka mitano wakati habari kuhusu Sauli na Yonathani zilipofika kutoka Yezreeli,^e mlezi wake akambeba na kukimbia, lakini alipokuwa akikimbia kwa woga, mwana huyo alianguka na kulemaa. Mwana huyo alitwa Mefiboshethi.^f

5 Rekabu na Baana, wana wa Rimoni Mbeerothi, walienda nyumbani kwa Ish-boshethi mchana wakati wa jua kali, alipokuwa akipumzika aduhuri. **6** Wakaingia nyumbani mwake kana kwamba wamekuja kuchukua ngano, wakampiga tumboni; kisha Rekabu na Baana^g ndugu yake wakakimbia. **7** Walipoingia nyumbani, alikuwa amelala kitandani mwake katika chumba chake cha kulala, wakampiga na kumuua, kisha wakamkata kichwa. Halafu wakakichukua na kutembea usiku kucha kwenye barabara inayoenda Araba. **8** Wakamletea Daudi kichwa cha Ish-boshethi^h huko Hebroni na kumwambia mfalme: "Ndicho hiki kichwa cha Ish-boshethi mwana wa Sauli adui yakoⁱ aliyetaka kukuua.^j Leo hii Yeho-

4:4 *Au "kiwete."

SURA YA 4

a Yos 9:17
Yos 18:21, 25

b Ne 11:31, 33

c 1Sa 20:16

d 2Sa 9:3

e 1Sa 29:1, 11

f 2Sa 9:13
1Nya 8:34

g 2Sa 4:2

h 2Sa 2:10

i 1Sa 18:28, 29

j 1Sa 18:10, 11
1Sa 20:1, 33
1Sa 23:15

Safu ya 2

a 1Sa 24:12
1Sa 26:25
2Sa 12:7
Zb 34:7

b 2Sa 1:2, 4

c 2Sa 1:13-15

d Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:16, 30

e Zb 55:23

f Kum 21:22

SURA YA 5

g 2Sa 2:1, 11
1Nya 12:23

h 1Nya 11:1-3

i 1Sa 18:13
1Sa 25:28

j Mwa 49:10
1Sa 16:1
1Sa 25:30
2Sa 6:21
2Sa 7:8
1Nya 28:4
Zb 78:71

va amekulipizia kisasi bwana wangu mfalme dhidi ya Sauli na wazao wake."

9 Hata hivyo, Daudi akamjibu hivi Rekabu na Baana ndugu yake, wana wa Rimoni Mbeerothi: "Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, aliyenikoa* kutoka katika taabu zote,^a **10** mtu fulani aliponiambia, 'Sauli amekufa,'^b akifikiri ananiletea habari nje-ma, nilimkamata na kumuua^c kule Siklagi. Hayo ndiyo malipo ya mjumbe aliyopokea kutoka kwangu! **11** Itakuwaje wakati wanaume waovu wamemua mtu mwadilifu nyumbani mwake mwenyewe akiwa katika kitanda chake? Kwa nini nisidai damu yake kutoka mikononi mwenu^d na kuwaangamiza kutoka duniani?"

12 Kisha Daudi akawaamuru vijana wake wawaue.^e Wakawakata mikono na miguu yao na kuwatundika^f kando ya kidimbwi kilicho Hebroni. Lakini wakachukua kichwa cha Ish-boshethi na kukizika katika kaburi la Abneri huko Hebroni.

5 Baada ya muda makabila yote ya Israeli yakaja kwa Daudi huko Hebroni^g na kusema: "Tazama! Sisi ni mfupa wako na nyama yako.^{*h} **2** Zamani, Sauli alipokuwa mfalme wetu, ni wewe uliyewaongoza Waisraeli vitani.^{*i} Na Yehova alikuambia hivi: 'Utawachunga watu wangu Waisraeli, nawe utakuwa kiongozi wa Israeli.'^j **3** Basi wazee wote wa Israeli wakaja kwa mfalme

4:9 *Au "aliyeikomboa nafsi yangu."
5:1 *Tnn., "Tuna uhusiano wa damu nawe." 5:2 *Tnn., "uliyekuwa ukiwama nje na kuwaingiza ndani Waisraeli."

huko Hebroni, na Mfalme Daudi akafanya agano nao^a huko Hebroni mbele za Yehova. Kisha wakamtia mafuta Daudi awe mfalme wa Israeli.^b

4 Daudi alikuwa na umri wa miaka 30 alipowekwa kuwa mfalme, naye alitawala kwa miaka 40.^c **5** Huko Hebroni alitawala Yuda kwa miaka 7 na miezi 6, na huko Yerusalemu^d alitawala Israeli yote na Yuda kwa miaka 33. **6** Mfalme na wanaume wake wakaenda Yerusalemu kuwashambulia Wayebusi^e waliokuwa wakiishi nchini. Walimdhihakia Daudi wakisema: "Hutaingia humu kamwe! Hata vipofu na vilema watakufukuza." Hivi ndivyo walivyofikiri: 'Daudi hataingia humu kamwe.'^f **7** Hata hivyo, Daudi akaiteka ngome ya Sayuni, ambayo sasa ni Jiji la Daudi.^g **8** Basi siku hiyo Daudi akasema: "Wale wanao-washambulia Wayebusi wanaswa kupitia kwenye mferaji wa maji ili wawaue 'vilema na vipofu,' wanaomchukia Daudi!"^{*} Ndiyo sababu watu wanasema: "Vipofu na vilema hawataingia nyumbani." **9** Kisha Daudi akaanza kukaa katika ngome hiyo, nayo ikaitwa^{*} Jiji la Daudi; na Daudi akaanza kujenga pande zote kuanzia kwenye Kilima^h kuja ndani.ⁱ **10** Kwa hiyo Daudi akawa mkuu zaidi na zaidi,^j na Yehova Mungu wa majeshi alikuwa pamoja naye.^k

11 Mfalme Hiram^l wa Tiro akawatuma wajumbe kwa Daudi, na kupeleka mbaao za mierezi,^m maseremala,

5:8 *Au "wanaoichukia nafsi ya Daudi."
5:9 *Au labda, "naye akaita." *Au "Milo." Neno la Kiebrania linalomaanisha "jaza."

SURA YA 5

- a 2Fa 11:17
b 1Sa 16:13
2Sa 2:4
Mdo 13:22
c 1Nya 29:26, 27
d Mwa 14:18
e Kut 23:23
Yos 15:63
Amu 1:8, 21
f 1Nya 11:4-6
g 1Fa 2:10
Ne 12:37
h 1Fa 9:15, 24
1Fa 11:27
2Nya 32:5
i 1Nya 11:7-9
j 1Sa 16:13
2Sa 3:1
k 1Sa 17:45
l 1Fa 5:1, 8
m 2Nya 2:3

Safu ya 2

- a 2Sa 7:2
1Nya 14:1, 2
b 2Sa 7:16
Zb 41:11
Zb 89:21
c Zb 89:27
d 1Fa 10:9
2Nya 2:11
e 2Sa 15:16
f 1Nya 3:5-9
1Nya 14:3-7
g Lu 3:23, 31
h 2Sa 12:24
i 2Sa 5:3
j Zb 2:2
k 1Sa 22:1, 5
1Sa 24:22
2Sa 23:14
1Nya 14:8
l Yos 15:8, 12
1Nya 11:15
1Nya 14:9
m Hes 27:21

- n 1Nya 14:10-12
o 2Sa 22:41
p Isa 28:21

na waashi wa kujenga kuta, nao wakaanza kumjengea Daudi nyumba.^{*a} **12** Na Daudi akajua kwamba Yehova alikuwa amemwimarisha kabisa kuwa mfalme wa Israeli^b na kwamba alikuwa amekweza ufalme wake^c kwa ajili ya watu Wake Waisraeli.^d

13 Baada ya kutoka Hebroni, Daudi alichukua masuria^e na wake zaidi huko Yerusalemu, nao wakanzalia Daudi wana na mabinti zaidi.^f **14** Haya ndiyo majina ya watoto wake waliozaliwa Yerusalemu: Shamua, Shobabu, Nathani,^g Sulemani,^h **15** Ibhari, Elishua, Nefegi, Yafia, **16** Elishama, Eliada, na Elifeleti.

17 Wafilisti waliposikia kwamba Daudi alikuwa ametiwa mafuta kuwa mfalme wa Waisraeli wote,ⁱ Wafilisti wote wakapanda kuja kumtafuta Daudi.^j Daudi aliposikia jambo hilo, akashuka kuingia ndani ya ngome.^k **18** Kisha Wafilisti wakaja na kuenea katika Bonde la^{*} Refaimu.^l **19** Daudi akamuuliza Yehova:^m "Je, ni-pande kwenda kuwashambulia Wafilisti? Je, utawatia mikononi mwangu?" Ndipo Yehova akamwambia Daudi: "Panda uende, nami hakika nitawatia Wafilisti mikononi mwako."ⁿ

20 Basi Daudi akaenda Baalperasimu na kuwaua huko. Ndipo akasema: "Yehova amewapasua na kuwapita^o maadui wangu mbele yangu, kama ufa uliopasuliwa na maji." Ndiyo sababu alipaita mahali hapo Baalperasimu.^{*p} **21** Wafilisti wakaacha sanamu zao

5:11 *Au "jumba la mfalme." **5:18** *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya." **5:20** *Maana yake "Bwana Anayepasua na Kupita."

hapo, na Daudi na wanaume wake wakazichukua na kwenenda nazo.

22 Baadaye Wafilisti waka-ja tena na kuenea katika Bonde la* Refaimu.^a **23** Daudi akamwomba Yehova ushauri, lakini Akasema: “Usipande moja kwa moja. Badala yake, zunguka nyuma yao, uwashambulie mbele ya vichaka vya mibaka. **24** Na utakaposikia sauti ya watu wakipiga mwendo juu ya vichaka vya mibaka, tenda bila kusita, kwa sababu mimi Yehova nitakuwa nimetangulia mbele yako kuliua jeshi la Wafilisti.” **25** Basi Daudi akafanya kama Yehova alivyomwamuru, akawaua Wafilisti^b kuanzia Geba^c mpaka Gezeri.^d

6 Daudi akawakusanya tena wanajeshi wote walio bora wa Israeli, wanaume 30,000. **2** Kisha Daudi na wanaume wote waliokuwa pamoja naye wakaondoka kwenda Baale-yuda ili kuleta Sanduku la Mungu wa kweli^e kutoka huko, ambalo mbele yake watu hulisifu jina la Yehova wa majeshi,^f anayeketi kwenye kiti cha ufalme juu ya* makerubi.^g **3** Hata hivyo, wakaweka Sanduku la Mungu wa kweli juu ya gari jipya la kukotwa^h ili walisafirisha kutoka katika nyumba ya Abinadabu,ⁱ iliyokuwa kwenye kilima; na Uza na Ahio, wana wa Abinadabu, walikuwa wakiliongoza gari hilo jipya.

4 Basi wakalisafirisha Sanduku la Mungu wa kweli kutoka katika nyumba ya Abinadabu iliyokuwa kwenye kili-

5:22 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”
6:2 *Au labda, “katikati ya.”

SURA YA 5

a Yos 15:8,12
1Nya 11:15
1Nya 14:13-17

b Law 26:7

c Yos 18:21, 24

d Yos 16:10

SURA YA 6

e 1Sa 7:2
1Fa 8:1
1Nya 13:1-5

f Kum 20:4
1Sa 1:3
1Nya 17:24

g Kut 25:22
1Sa 4:4
1Nya 13:6-11
Zb 80:1

h Kut 25:14
Hes 7:9
Yos 3:14

i 1Sa 7:1

Safu ya 2

a 1Sa 10:5

b Kut 15:20

c Zb 150:3-5

d Hes 4:15
1Nya 15:2

e Law 10:1, 2
1Sa 6:19

f Met 11:2

g 1Sa 6:20
Zb 119:120

h 1Nya 13:12-14

i 2Sa 5:7

j 1Nya 15:25

k Mwa 30:27
Mwa 39:5

ma, na Ahio alikuwa aki-tembea mbele ya Sanduku hilo. **5** Daudi na nyumba yote ya Israeli walikuwa wakisherehekea mbele za Yehova kwa ala za kila aina zilizotengenezwa kwa mbaao za mberoshi, vinubi, vinanda vinginevyo,^a matari,^b matasa, na matoazi.^c **6** Lakini walipofika kwenye uwanja wa kupuria wa Nakoni, Uza akau-nyoosha mkono wake haraka na kulikamata Sanduku la Mungu wa kweli,^d kwa sababu ng'ombe walikuwa karibu kuliangusha. **7** Ndipo hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Uza, na Mungu wa kweli akamuua^e papo hapo kwa sababu ya tendo lake lisilo la heshima,^f akafa hapo karibu na Sanduku la Mungu wa kweli. **8** Lakini Daudi akakasirika kwa sababu hasira kali ya Yehova ili waka dhidi ya Uza; na tangu siku hiyo mahali hapo panaitwa Peres-uzi.* **9** Basi Daudi akamwogopa Yehova^g siku hiyo na kusema: “Sanduku la Yehova linawezaje kuja kwangu?”^h **10** Daudi hakutaka kuleta Sanduku la Yehova mahali alipokuwa katika Jiji la Daudi.ⁱ Badala yake, Daudi aliagiza lipelekwe katika nyumba ya Obed-edomu,^j Mgathi.

11 Sanduku la Yehova likaendelea kukaa katika nyumba ya Obed-edomu Mgathi kwa miezi mitatu, na Yehova akazidi kumbariki Obed-edomu na nyumba yake yote.^k **12** Mfalme Daudi akaambiwa hivi: “Yehova ameibariki nyumba ya Obed-edomu na vitu vyake vyote kwa sababu ya

6:8 *Maana yake “Ghadhabu Dhidi ya Uza.”

Sanduku la Mungu wa kweli." Basi Daudi akaenda kuli-chukua Sanduku la Mungu wa kweli kutoka katika nyumba ya Obed-edomu na kulipandisha kwa shangwe katika Jiji la Daudi.^a **13** Wale waliobeba^b Sanduku la Yehova walipokuwa wamepiga hatua sita, Daudi alitoka dhabihu ya ng'ombe dume na mnyama aliye-noneshwa.

14 Daudi alikuwa akicheza dansi huku na huku mbele za Yehova kwa nguvu zake zote; na wakati wote huo Daudi alikuwa amevaa* efodi ya kitani.^c **15** Daudi na nyumba yote ya Israeli walikuwa wakilipandisha Sanduku^d la Yehova kwa kelele za shangwe^e na sauti ya pembe.^f **16** Lakini Sanduku la Yehova lili-pingia katika Jiji la Daudi, Mikali,^g binti ya Sauli, akaangalia chini kupitia dirishani, akamwona Mfalme Daudi akirukaruka na kucheza dansi huku na huku mbele za Yehova; naye akaanza kumdhara-rau moyoni mwake.^h **17** Basi wakaliingiza ndani Sanduku la Yehova na kuliweka mahali pake ndani ya hema ambalo Daudi alikuwa amepiga ili aliweke humo.ⁱ Kisha Daudi akatoa dhabihu za kuteketezwa^j na dhabihu za ushirika^k mbele za Yehova.^l **18** Daudi alipomaliza kutoa dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za ushirika, akawabariki watu katika jina la Yehova wa majeshi. **19** Pia, akawagawia watu wote, umati wote wa Waisraeli, kila mwanamume na mwanamke mkate wa mviringo, keki ya tende, na keki ya zabibu kavu, halafu

6:14 *Tnn., "amejifunga."

SURA YA 6

a 1Nya 15:25, 26
Zb 24:7
Zb 68:24

b Hes 4:15
Hes 7:9
Yos 3:3
1Nya 15:2, 15

c 1Nya 15:27, 28

d Kut 37:1
Zb 132:8

e 1Nya 15:16

f Zb 150:3

g 1Sa 14:49
1Sa 18:20, 27
2Sa 3:14

h 1Nya 15:29

i 1Nya 15:1

j Law 1:3

k Law 3:1

l 1Nya 16:1-3

Safu ya 2

a 1Sa 18:27

b Kut 22:28

c 1Sa 13:13, 14
1Sa 15:27, 28
1Sa 16:1, 12

d 1Sa 14:49
2Sa 6:16

SURA YA 7

e 1Nya 17:1

f 2Sa 12:1
1Nya 29:29

g 2Sa 5:11

h 2Sa 6:17

i 1Fa 8:17
1Nya 17:2
1Nya 22:7

watu wote wakaenda zao, kila mmoja nyumbani kwake mwenyewe.

20 Daudi aliporudi ili kuwabariki watu wa nyumba yake mwenyewe, Mikali, binti ya Sauli^a akatoka nje kumpokea Daudi. Mikali akasema: "Mfalme wa Israeli amejitukuza kwelikweli leo kwa kujifunua leo mbele ya macho ya vijakazi wa watumishi wake, kama tu mtu asiye na akili anavyojifunua waziwazi!"^b **21** Ndipo Daudi akamwambia Mikali: "Nilikuwa nikisherehekea mbele za Yehova, aliyenichagua mimi badala ya baba yako na nyumba yake yote na ambaye aliniweka mimi kuwa kiongozi wa watu wa Yehova, Waisraeli.^c Kwa hiyo, nita-sherehekea mbele za Yehova, **22** nami nitajinyenyekeza zaidi hata kuliko nilivyofanya na kuwa mdogo hata machoni pangu mwenyewe. Lakini nitatukuzwa na hao vijakazi uliowataja." **23** Basi Mikali,^d binti ya Sauli, hakuwa na watoto mpaka siku alipokufa.

7 Mfalme alipoanza kuishi katika nyumba yake mwenyewe*^e na baada ya Yehova kumpumzisha kutokana na maadui wake wote waliomzwunguka, **2** mfalme alimwambia hivi nabii Nathani:^f "Mimi hapa ninaishi katika nyumba ya mierezi^g huku Sanduku la Mungu wa kweli liki-kaa katikati ya vitambaa vya mahema."^h **3** Nathani akamwambia mfalme: "Nenda ufanye jambo lolote lililo moyoni mwako, kwa sababu Yehova yuko pamoja nawe."ⁱ

7:1 *Au "jumba lake mwenyewe la mfalme."

4 Usiku huohuo, neno hili la Yehova likamjia Nathani: 5 “Nenda ukamwambie mtumishi wangu Daudi, ‘Yehova anasema hivi: “Je, utanijengea nyumba nikae ndani yake?’” 6 Kwa maana sijakaa ndani ya nyumba tangu siku nilipowatoa watu wa Israeli huko Misiri mpaka leo,^b bali nimekuwa nikihama* huku na kule katika hema na katika hema la ibada.^c 7 Wakati wote nilipotembea na Waisraeli wote,* je, niliwahi wakati wowote kumuuliza kiongozi yeyote wa kabila la Israeli niliyemweka awachunge watu wangu Waisraeli, ‘Kwa nini hukunijengea nyumba ya mierezi?’” 8 Sasa mwambie hivi mtumishi wangu Daudi: ‘Yehova wa majeshi anasema hivi: “Nilikutoa malishoni, ili usiendeleo kuchunga kondoo,^d uwe kiongozi wa watu wangu Waisraeli.^e 9 Nami nitakuwa pamoja nawe popote utakapoenda,^f nami nitawaangamiza maadui wako wote kutoka mbele yako;^g nami nitafanya jina lako liwe maarufu^h kama jina la watu maarufu duniani. 10 Nitachagua mahali kwa ajili ya watu wangu Waisraeli na kuwaweka humo, nao wataishi humo na hawatasumbuliwa tena; na watu waovu hawatawakandamiza tena kama walivyofanya zamani,ⁱ 11 tangu siku nilipowaweka waamuzi/ juu ya watu wangu Waisraeli. Nami nitakupumzisha kutokana na maadui wako wote.^k ““Pia, Yehova amekuambia kwamba Yehova atakujengea nyumba.*^l 12 Siku zako zi-

7:6 *Tnn., “nikitembea.” 7:7 *Tnn., “wana wote wa Israeli.” 7:11 *Au “ukoo wa kifalme.”

SURA YA 7

a 1Fa 5:3
1Fa 8:17-19
1Nya 17:4-6
1Nya 22:7, 8

b Yos 18:1

c Kut 40:18, 34

d 1Sa 16:11

e 2Sa 5:2
1Nya 17:7-10
1Nya 28:4
Zb 78:70, 71

f 1Sa 18:14
2Sa 5:10

g 2Sa 22:1
Zb 18:37

h 1Nya 14:2, 17

i Amu 2:14
Zb 89:20, 22

j Amu 2:16

k Kum 25:19

l 1Fa 2:24
Zb 89:4

Safu ya 2

a 1Fa 2:1

b Mwa 49:10
1Fa 8:20
1Nya 17:11-14
Zb 132:11

Isa 9:7
Isa 11:1
Mt 21:9
Mt 22:42
Lu 1:32, 33
Yoh 7:42
Mdo 2:30

c 1Fa 5:5
1Fa 6:12
Zek 6:12, 13

d 1Fa 1:37
1Nya 22:10
1Nya 28:7
Zb 89:4, 36

e 1Nya 28:6
Mt 3:17
Ebr 1:5

f Zb 89:30, 32
Yer 52:3

g 1Sa 15:23, 26

h Zb 45:6
Zb 89:36
Da 2:44
Ebr 1:8
Ufu 11:15

i 1Nya 17:15

j 1Nya 17:16-22

takapokwisha^a nawe ufe na kuzikwa pamoja na mababu zako, ndipo nitakapomwinua mzao wako* baada yako, mwana wako mwenyewe,[#] nami nitauimarisha kabisa ufalme wake.^b 13 Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili ya jina langu,^c nami nitakiiimarisha kabisa kiti cha ufalme wake milele.^d 14 Nita kuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu.^e Atakapokosea, nitamkaripia kwa fimbo ya wanadamu na kwa viboko vya wana wa binadamu.*^f 15 Upendo wangu mshikamanifu hautaondolewa kwake kama nilivyoondoa kwa Sauli,^g niliyemwondoa kutoka mbele yako. 16 Nyumba yako na ufalme wako utakuwa salama milele mbele yako; kiti chako cha ufalme kitaimarishwa kabisa milele.*^h

17 Nathani akamwambia Daudi maneno hayo yote na maono hayo yote.ⁱ

18 Ndipo Mfalme Daudi akaingia na kuketi mbele za Yehova na kusema: “Mimi ni nani, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova? Na nyumba yangu ni nini hivi kwamba umenileta mpaka hapa nilipofika?^j 19 Na kana kwamba hilo halitoshi, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, unasema pia kwamba nyumba yangu mimi mtumishi wako itadumu kwa muda mrefu; na haya ni maagizo* kwa wanadamu wote, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. 20 Mimi mtumishi wako Daudi nitakwambia nini zaidi

7:12 *Tnn., “mbegu yako.” #Tnn., “yule atakayetoka katika viungo vyako vya ndani.” 7:14 *Au labda, “Adamu.” 7:19 *Au “na hii ni sheria.”

wakati unanijua vizuri sana,^a Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova? **21** Kwa ajili ya neno lako na kupatana na moyo wako* umetenda mambo haya yote makuu na kunifunulia mimi mtumishi wako.^b **22** Ndiyo sababu wewe kwa kweli ni mkuu,^c Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. Hakuna aliye kama wewe,^d na hakuna Mungu ila wewe;^e mambo yote tuliyosikia kwa masikio yetu yanathibitisha jambo hilo. **23** Na kuna taifa gani lingine duniani lililo kama watu wako Waisraeli?^f Wewe Mungu ulienda na kuwakomboa wakiwa watu wako,^g ukajijengea jina,^h kwa kufanya mambo makuu na yenye kuogopesha kwa ajili yao.ⁱ Uliyafukuza mataifa na miungu yao kwa ajili ya watu wako, ambao uliwa-komboa kutoka Misri kwa ajili yako mwenyewe. **24** Uliwaimarisha watu wako Waisraeli ili wawe watu wako milele;^j na wewe, Ee Yehova, umekuwau Mungu wao.^k

25 "Sasa, Ee Yehova Mungu, timiza ahadi uliyotoa kuni-husu mimi mtumishi wako na nyumba yangu milele, na ufanye kama ulivyoahidi.^l **26** Jina lako na likwezwe milele,^m ili watu waseme, 'Yehova wa majeshi ni Mungu wa Israeli,' na nyumba yangu mimi mtumishi wako Daudi na iimarishwe kabisa mbele zako.ⁿ **27** Kwa maana wewe, Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, umenifunulia mimi mtumishi wako ukisema, 'Nitakujengea nyumba.'^o Ndiyo sababu mimi mtumishi wako nina

7:21 *Au "kulingana na mapenzi yako."
7:27 *Au "ukoo wa kifalme."

SURA YA 7

- a 1Sa 16:7
Zb 17:3
b Zb 25:14
c Kum 3:24
1Nya 16:25
d Kut 15:11
Zb 83:18
e Kum 4:35
f Kum 4:7
Zb 147:19, 20
g Kut 3:8
Kut 19:5
Isa 63:9
h Kut 9:16
i Kum 10:21
j Kum 26:18
k Kut 15:2
l 1Nya 17:23-27
Zb 89:20, 28
m 1Nya 29:11
Zb 72:19
Mt 6:9
Yoh 12:28
n Isa 9:7
Yer 33:22
o 2Sa 7:11

Safu ya 2

- a Hes 23:19
Zb 89:35
Zb 132:11
Yoh 17:17
b Zb 89:20, 36
Zb 132:12
c 2Sa 22:51
Zb 72:17

SURA YA 8

- d Yos 13:2, 3
2Sa 21:15
e 1Nya 18:1
f Hes 24:17
Amu 3:29
1Sa 14:47
Zb 60:8
g Kum 23:3-6
h 2Fa 3:4
1Nya 18:2
i 2Sa 10:6
1Fa 11:23
Zb 60:Uta
j Mwa 15:18
Kut 23:31
1Fa 4:21
1Nya 18:3, 4
k Kum 17:16
Zb 20:7
Zb 33:17
l Isa 7:8
m 1Nya 18:5, 6

ujasiri wa* kutoa sala hii kwako. **28** Na sasa, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, wewe ndiye Mungu wa kweli, na maneno yako ni kweli,^a nawe umeniahidi mimi mtumishi wako mambo hayo mema. **29** Basi na ufurahie kuibariki nyumba yangu mimi mtumishi wako, na idumu milele mbele zako;^b kwa sababu wewe, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, umeahidi, na kwa baraka yako, nyumba yangu mimi mtumishi wako na ibarikiwe milele.^c

8 Baadaye, Daudi aliwashinda Wafilisti^d na kuwatii-sha,^e akachukua jiji la Methegama kutoka mikononi mwa Wafilisti.

2 Akawashinda Wamoabu^f na kuwaamuru walale chini ardhini, naye akawapima kwa kamba. Alipima safu mbili za watu ambao wangeuawa, na safu moja nzima ya watu ambao hawangeuawa.^g Wamoabu wakawa watumishi wa Daudi na kumletea ushuru.^h

3 Daudi alimshinda Hadadezeri mwanza wa Rehobu mfalme wa Sobaⁱ mfalme huyo alipokuwa akienda kurudisha mamlaka yake katika eneo la Mto Efrati.^j **4** Daudi akawateka wapanda farasi 1,700 na wanajeshi wake 20,000 wanaotembea kwa miguu. Kisha Daudi akawakata farasi wote mishipa ya miguu isipokuwa farasi 100 waliokokota magari.^k

5 Wasiria wa Damasko^l walipokuja kumsaidia Mfalme Hadadezeri wa Soba, Daudi aliwaua Wasiria 22,000.^m

6 Halafu Daudi akaweka ka-

7:27 *Tnn., "nimepata moyo wa."

mbi za kijeshi kule Siria ya Damasko, na Wasiria wakawa watumishi wa Daudi na kumletea ushuru. Yehova alimpa Daudi ushindi* popote alipoenda.^a **7** Isitoshe, Daudi alichukua ngao za mviringo za dhahabu kutoka kwa watumishi wa Hadadezeri na kuzileta Yerusalemu.^b **8** Mfalme Daudi alichukua shaba nyingi sana kutoka Beta na Berothai, majiji ya Hadadezeri.

9 Basi Mfalme Toi wa Hamathi^c akasikia kwamba Daudi alikuwa amelishinda jeshi lote la Hadadezeri.^d **10** Kwa hiyo Toi akamtuma Yoramu mwana wake kwa Mfalme Daudi ili amjulie hali na kumpongeza kwa sababu alikuwa amepigana na Hadadezeri na kumshinda (kwa maana mara nyingi Hadadezeri alimshambulia Toi); na Yoramu alimletea Daudi vitu vya fedha, dhahabu, na shaba. **11** Mfalme Daudi akavitakasa vitu hivyo ili viwe vya Yehova, pamoja na fedha na dhahabu aliyotakasa kutoka kwa mataifa yote aliyokuwa ameyashinda.^e **12** kutoka Siria na kutoka Moabu,^f kutoka kwa Waamoni, Wafilisti,^g Waamaleki,^h na kutoka katika nyara za Hadadezeriⁱ mwana wa Rehobu mfalme wa Soba. **13** Pia Daudi alijijengea jina aliporudi baada ya kuwaua Waedomu 18,000 katika Bonde la Chumvi.^j **14** Aliweka kambi za kijeshi huko Edomu. Aliweka kambi za kijeshi katika nchi yote ya Edomu, na Waedomu wote wakawa watumishi wa Daudi.^k Yehova alimpa Daudi ushindi* popote alipoenda.^l

8:6, 14 *Au "wokovu."

SURA YA 8

a Kum 7:24
2Sa 8:14

b 1Nya 18:7, 8

c 2Fa 14:28

d 1Nya 18:9-11

e Yos 6:19
1Fa 7:51
1Nya 22:14
1Nya 26:27

f 2Sa 8:2

g 2Sa 8:1

h 1Sa 30:18

i 2Sa 8:7

j 1Nya 18:12, 13
Zb 60:Uta

k Mwa 25:23, 26
Mwa 27:29, 37
Hes 24:18

l Zb 60:12

Safu ya 2

a 2Sa 5:3, 5

b 1Nya 18:14-17

c 1Fa 3:6

d 2Sa 20:23
1Nya 11:6

e 2Sa 20:24
1Fa 4:3

f 2Sa 15:27
1Nya 6:8
1Nya 24:3

g 2Sa 23:20
1Fa 1:44
1Fa 2:35

h 2Sa 15:18
2Sa 20:7

SURA YA 9

i 1Sa 18:1, 3
1Sa 20:15, 42

j 2Sa 16:1
2Sa 19:17

k 2Sa 4:4
2Sa 9:13
2Sa 19:26

l 2Sa 17:27-29

15 Daudi akaendelea kutawala Israeli yote,^a naye aliwatawala watu wake wote^b kwa haki na uadilifu.^c **16** Yoabu^d mwana wa Seruya alikuwa mkuu wa jeshi, na Yehoshafati^e mwana wa Ahiludi alifanya kazi ya kuweka kumbukumbu. **17** Sadoki^f mwana wa Ahitubu na Ahimeleki mwana wa Abiathari walikuwa makuhani, na Seraya alikuwa mwandishi. **18** Benaya^g mwana wa Yehoyada aliwasimamia Wakerethi na Wapelethi.^h Na wana wa Daudi walikuwa wahudumu wakuu.*

9 Kisha Daudi akauliza: "Je, kuna yeyote aliyebaki katika nyumba ya Sauli ninayeweza kumtendea kwa upendo mshikamanifu kwa ajili ya Yonathani?"ⁱ **2** Basi kulikuwa na mtumishi wa nyumba ya Sauli aliyeitwa Siba.^j Kwa hiyo wakamwita aje kwa Daudi, na mfalme akamuuliza: "Je, wewe ni Siba?" Akajibu: "Ni mimi mtumishi wako." **3** Mfalme akaendelea kumuuliza: "Je, kuna yeyote aliyebaki katika nyumba ya Sauli ninayeweza kumtendea kwa upendo mshikamanifu wa Mungu?" Siba akamjibu hivi mfalme: "Bado kuna mwana mmoja wa Yonathani; amelemaa miguu yote miwili."^k **4** Mfalme akamuuliza: "Yuko wapi?" Siba akamjibu mfalme: "Yuko katika nyumba ya Makiri^l mwana wa Amieli kule Lo-debari."

5 Mara moja Mfalme Daudi akaagiza aletwe kutoka katika nyumba ya Makiri mwana wa Amieli kule Lo-debari.

8:18 *Tnn., "walikuwa makuhani." 9:3 *Au "ni kiwete."

6 Mefiboshethi mwana wa Yonathani mwana wa Sauli alipofika mbele ya Daudi, mara moja alianguka chini kifudufudi na kumwinamia. Daudi akasema: "Mefiboshethi!" naye akajibu: "Mimi hapa, mtumishi wako." 7 Daudi akamwambia: "Usiogoje, kwa maana hakika nitakutendea kwa upendo mshikamanifu^a kwa ajili ya Yonathani baba yako, nami nitakurudishia ardhi yote ya Sauli babu yako, nawe utakula chakula* mezani pangu sikuzote."^b

8 Basi akainama na kusema: "Mimi mtumishi wako ni nani, hivi kwamba umenitendea kwa fadhili* mbwa mfuc^c kama mimi?" 9 Sasa mfalme akaagiza Siba mtumishi wa Sauli aitwe, akamwambia: "Kila kitu ambacho kilikuwa cha Sauli na nyumba yake yote ninampa mjukuu wa bwana wako.^d 10 Wewe na wana wako na watumishi wako mtamlimia shamba lake, nanyi mtayakusanya mavuno ya shamba hilo ili watu wa nyumbani mwa mjukuu wa bwana wako wapate chakula. Lakini Mefiboshethi, mjukuu wa bwana wako, atakula chakula mezani pangu sikuzote."^e

Siba alikuwa na wana 15 na watumishi 20.^f 11 Ndipo Siba akamwambia mfalme: "Mimi mtumishi wako nitafanya mambo yote ambayo bwana wangu mfalme unaniamuru mimi mtumishi wako nifanye." Basi Mefiboshethi akawa akila kwenye meza ya Daudi* kama mmoja wa wana wa mfalme. 12 Sasa Mefiboshethi pia ali-

9:7 *Tnn., "mkate." 9:8 *Tnn., "umegeuza uso wako kuelekea." 9:11 *Au labda, "meza yangu."

SURA YA 9

a Met 11:17

b 2Sa 19:28
Met 11:25

c 1Sa 24:14

d 2Sa 9:1
2Sa 16:4
2Sa 19:29

e 2Sa 19:28

f 2Sa 19:17

Safu ya 2

a 1Nya 8:34
1Nya 9:40b 2Sa 9:7
2Sa 19:28

c 2Sa 4:4

SURA YA 10

d Mwa 19:36, 38
Amu 10:7
Amu 11:12, 33
1Sa 11:1

e 1Nya 19:1-5

f Law 19:27

g Yos 18:21

kuwa na mtoto mdogo wa kiume aliyeitwa Mika;^a na watu wote walioishi katika nyumba ya Siba wakawa watumishi wa Mefiboshethi. 13 Naye Mefiboshethi aliishi Yerusalemu kwa maana sikuzote alikula mezani pa mfalme;^b na miguu yake ilikuwa imelemaa.^c

10 Baadaye mfalme wa Waamoni^d akafa, na Hanuni mwanawe akawa mfalme baada yake.^e 2 Ndipo Daudi akasema: "Nitamtendea kwa upendo mshikamanifu Hanuni mwana wa Nahashi kama baba yake alivyonitendea kwa upendo mshikamanifu." Basi Daudi akawatuma watumishi wake ili wamfariji baada ya kufiwa na baba yake. Lakini watumishi wa Daudi walipofika katika nchi ya Waamoni, 3 wakuu wa Waamoni wakamwambia Hanuni bwana wao: "Je, unafikiri kwamba Daudi anawatuma wafariji kwako ili kumheshimu baba yako? Je, Daudi hajawatuma watumishi wake ili kulichunguza jiji lote na kulipeleleza na kuliteka?" 4 Kwa hiyo Hanuni akawachukua watumishi wa Daudi, akawanyoa nusu ya ndevu zao,^f akakata nguo zao katika tiki kwenye matako na kuwafukuza. 5 Daudi alipoambiwa habari hiyo, mara moja akawatuma wanaume fulani wainde kukutana nao, kwa sababu watumishi hao walikuwa wameaibishwa sana; mfalme akawaambia: "Kaeni Yeriko^g mpaka ndevu zenu zitakapoota, kisha mrudi."

6 Baada ya muda Waamoni wakaona kuwa wananuka mbele ya Daudi, kwa hiyo wawatuma wajumbe waende kuwakodi Wasiria wa Beth-

rehobu^a na Wasiria wa Soba,^b wanajeshi 20,000 wanaote-mbea kwa miguu; na mfalme wa Maaka^c akiwa na wanaume 1,000; na kutoka Ishtobu,* wanaume 12,000.^d **7** Daudi aliposikia habari hizo, akamtu-ma Yoabu na jeshi lote, kutia ndani mashujaa wake hodari zaidi.^e **8** Nao Waamoni wakato-ka na kujipanga kivita kwenye lango la jiji huku Wasiria wa Soba na wa Rehobu, pamo-ja na Ishtobu* na Maaka, wa-kiwa peke yao uwanjani.

9 Yoabu alipoona kwamba anashambuliwa upande wa mbele na wa nyuma, aka-chagua baadhi ya wanajeshi bora katika Israeli na kuwapa-nga kivita ili wapigane na Wa-siria.^f **10** Wanaume walioba-ki aliwaweka chini ya usima-mizi wa* Abishai ndugu yake,^g ili awapange kivita kupigana na Waamoni.^h **11** Kisha aka-sema: "Kiwa Wasiria watanizi-di nguvu, basi mtaniokoa; la-kini Waamoni wakiwazidi ninyi nguvu, nitawaokoa. **12** Ni la-zima tuwe imara na jasiriⁱ kwa ajili ya watu wetu na kwa ajili ya majiji ya Mungu wetu, naye Yehova atafanya yaliyo mema machoni pake."^j

13 Kisha Yoabu na wana-ume wake wakasonga mbe-le kwenda kupigana vita na Wasiria, nao wakamkimbia.^k **14** Waamoni walipoona kwa-mba Wasiria wamekimbia, wa-kamkimbia Abishai na kuingia jijini. Baada ya Yoabu kupiga-na na Waamoni akarudi Yeru-salemu.

15 Wasiria walipoona kwa-mba wameshindwa na Wais-raeli, wakajikusanya tena.^l

10:6, 8 *Tnn., "wanaume wa Tobu."
10:10 *Tnn., "mikononi mwa."

SURA YA 10

a Hes 13:21

b 2Sa 8:5

c Yos 13:13

d 1Nya 19:6, 7

e 2Sa 23:8
1Nya 19:8, 9

f 1Nya 19:10-13

g 1Sa 26:6
2Sa 2:18
2Sa 23:18
1Nya 2:15, 16

h Hes 21:24

i Kum 31:6

j Zb 37:5
Zb 44:5
Met 29:25

k 1Nya 19:14, 15

l 1Nya 19:16

Safu ya 2

a 2Sa 8:3-5

b Mwa 15:18
Kut 23:31

c 1Nya 19:17-19

d Kum 20:1
Zb 18:37, 38e Mwa 15:18
Kum 20:10, 11

SURA YA 11

f 2Sa 12:26

g 1Nya 20:1

h 2Sa 12:24
1Fa 1:11

16 Basi Hadadezeri^a akaagi-za Wasiria kutoka katika eneo la Mto Efrati^b waletwe, nao wakaja Helamu, wakiiongozwa na Shobaki mkuu wa jeshi la Hadadezeri.

17 Daudi alipoambiwa ha-bari hiyo, akawakusanya mara moja Waisraeli wote, wa-kavuka Yordani na kufika He-lamu. Kisha Wasiria wakaji-panga kivita ili kwenda kupigana na Daudi.^c **18** Lakini Wasiria wakawakimbia Wais-raeli; na Daudi akawau Wasi-ria 700 wanaoendesha maga-ri ya vita na wapanda farasi 40,000, naye akampiga Shoba-ki mkuu wa jeshi, akafa huko.^d

19 Wafalme wote waliokuwa watumishi wa Hadadezeri walipoona kwamba wameshi-ndwa na Waisraeli, mara moja wakafanya amani na Waisrae-li, wakawa watumishi wao;^e na Wasiria wakaogopa kuwasai-dia tena Waamoni.

11 Mwanzoni mwa mwa-ka,* wakati ambapo wa-falme huenda vitani, Dau-di akamtuma Yoabu na watu-mishi wake pamoja na jeshi lote la Israeli kuwaangami-za Waamoni, nao wakalizingi-ra Raba,^f lakini Daudi aliba-ki Yerusalemu.^g

2 Jioni moja Daudi alia-mka kitandani akaenda ku-tembeatembea juu ya paa la nyumba ya mfalme.* Akiwa kwenye paa alimwona mwa-namke akioga, na mwanamke huyo alikuwa mrembo sana. **3** Daudi akamtuma mtu fulani aulize kuhusu mwanamke huyo, mtu huyo akamwa-mbia: "Ni Bath-sheba,^h binti ya

11:1 *Yaani, majira ya kuchipua. 11:2 *Au "jumba la mfalme."

Eliamu;^a mke wa Uria^b Mhiti.^c **4** Kisha Daudi akawatumajumbe wamlete.^d Basi akaja kwa Daudi, naye Daudi akalala naye.^e (Wakati huo mwanamke huyo alikuwa akijitakasa uchafu wake.)*^f Kisha, mwanamke huyo akarudi nyumbani kwake.

5 Mwanamke huyo akapata mimba, akatuma ujumbe huu kwa Daudi: "Nina mimba."

6 Ndipo Daudi akatuma ujumbe huu kwa Yoabu: "Mtume kwangu Uria Mhiti." Basi Yoabu akamtuma Uria kwa Daudi. **7** Uria alipofika, Daudi akamuuliza habari za Yoabu, habari kuhusu wanajeshi, na kuhusu vita. **8** Kisha Daudi akamwambia Uria: "Shuka uende nyumbani kwako ukapumzike."* Uria alipotoka nyumbani mwa mfalme, alipelekewa zawadi ya hisani kutoa kwa mfalme.[#] **9** Lakini Uria alilala kwenye mlango wa nyumba ya mfalme pamoja na watumishi wengine wote wa bwana wake, naye hakushuka kwenda nyumbani kwake. **10** Kwa hiyo Daudi akaambiwa: "Uria hakushuka kwenda nyumbani kwake." Ndipo Daudi akamuuliza Uria: "Umetoka safarini, sivyo? Kwa nini hukushuka kwenda nyumbani kwako?" **11** Uria akamjibu Daudi: "Sanduku la agano^g na wanaume wa Israeli na Yuda wanakaa katika vibanda, na bwana wangu Yoabu na watumishi wake wanapiga kambi uwanjani. Ninawezaje kwenda

11:4 *Huenda ni uchafu wa hedhi. **11:8** *Tnn., "ukanawe miguu yako." [#]Au "fungu la mfalme," yaani, fungu ambalo mwenyeji humtumia mgeni mheshiwa.

SURA YA 11

a 1Nya 3:5, 9

b 2Sa 23:8, 39
1Fa 15:5c Mwa 10:15
Kum 20:17

d Kut 20:14, 17

e Law 18:20
Law 20:10
Met 6:32
Ebr 13:4f Law 12:2
Law 15:19
Law 18:19g 2Sa 6:17
2Sa 7:2

Safu ya 2

a Law 15:16
1Sa 21:5b Zb 51:14
Met 3:29

c 2Sa 12:9

nyumbani kwangu kula na kunywa na kulala na mke wangu?^a Kwa hakika kama unavyoishi na kama ulivyo hai,* sitafanya hivyo!"

12 Basi Daudi akamwambia Uria: "Kaa hapa leo pia, na kesho nitakuruhusu uende." Kwa hiyo Uria akakaa Yerusalemu siku hiyo na siku iliyofuata. **13** Halafu Daudi akaagiza aitwe ili ale na kunywa pamoja naye, akamfanya alewe. Lakini jioni, Uria alienda kulala kitandani mwake pamoja na watumishi wa bwana wake, naye hakushuka kwenda nyumbani kwake. **14** Asubuhi Daudi akamwandikia Yoabu barua, akampa Uria aipeleke kwa Yoabu. **15** Katika barua hiyo, Daudi aliandika hivi: "Mwekeni Uria kwenye mstari wa mbele mahali ambapo vita ni vikali zaidi. Kisha mmwache na kurudi nyuma yake ili apigwe na kuuawa."^b

16 Yoabu alikuwa amelichunguza jiji kwa makini, basi alimweka Uria mahali ambapo alijua kuna wanajeshi mashujaa. **17** Wanauume wa jiji walipotoka nje na kupigana na Yoabu, baadhi ya watumishi wa Daudi waliuawa, na Uria Mhiti alikuwa miongoni mwa watu waliuawa.^c **18** Sasa Yoabu akampelekea Daudi habari zote za vita. **19** Alimpa mjumbe maagizo haya: "Utakapomaliza kumwambia mfalme habari zote za vita, **20** huenda mfalme atakasirika na ku-kuuliza, 'Kwa nini mlienda karibu sana na jiji kupigana? Je, hamkujua kwamba wata-

11:11 *Au "kama nafsi yako inavyoishi."

wapiga mishale kutoka juu ya ukuta? **21** Ni nani aliyemua Abimeleki^a mwana wa Yerubeshethi?^b Je, si mwanamke aliyemwangushia jiwe la juu la kusagia kutoka juu ya ukuta na kumuua kule Thebesi? Kwa nini mlienda karibu sana na ukuta?’ Kisha utamwambia, ‘Pia mtumishi wako Uria Mhiti amekufa.’”

22 Basi mjumbe huyo akaenda na kumwambia Daudi kila jambo ambalo Yoabu alimtuma amwambie. **23** Mjumbe huyo akamwambia Daudi: “Wanaume wao walituzidi nguvu, nao walitoka ili kutushambulia uwanjani; lakini tuliwarudisha nyuma mpaka kwenye lango la jiji. **24** Na wapiga mishale walikuwa wakiwapiga kwa mishale watumishi wako kutoka juu ya ukuta, na baadhi ya watumishi wako mfalme wakafa; mtumishi wako Uria Mhiti akafa pia.”^c **25** Ndipo Daudi akamwambia mjumbe huyo: “Mwambie hivi Yoabu: ‘Jambo hili lisikuhangaishe, kwa maana upanga humnyafua huyu na pia yule. Zidisheni mashambulizi dhidi ya jiji na mlisihnde.’^d Nawe umtie moyo.”

26 Mke wa Uria aliposikia kwamba Uria mume wake amekufa, akaanza kumwombolezea mume wake. **27** Mara tu kipindi cha kuomboleza kilipokwisha, Daudi akaagiza aletwe nyumbani kwake, akawa mke wake^e na kumzalia mwana. Lakini jambo ambalo Daudi alikuwa amefanya lilimchukiza sana* Yehova.^f

11:27 *Tnn., “lilikuwa jambo ovu machoni pa.”

SURA YA 11

a Amu 9:50-53

b Amu 6:32
Amu 7:1

c 2Sa 11:17

d 2Sa 12:26

e 2Sa 5:13
2Sa 12:9f Mwa 39:7-9
1Fa 15:5
Zb 5:6
Zb 11:4
Ebr 13:4

Safu ya 2

SURA YA 12

a 1Fa 1:8
1Nya 17:1
1Nya 29:29

b Zb 51:Uta

c 2Sa 5:13
2Sa 15:16

d 2Sa 11:3

e 2Sa 11:4

f Kum 6:13

g Kut 22:1

12 Kwa hiyo Yehova akamtuma Nathani^a kwa Daudi. Akafika kwake^b na kumwambia: “Kulikuwa na wanaume wawili katika jiji moja, mmoja alikuwa tajiri na mwingine maskini. **2** Yule mwanamume tajiri alikuwa na kondoo wengi sana na ng’ombe;^c **3** lakini yule mwanamume maskini hakuwa na chochote isipokuwa mwanakondoo mmoja jike mdogo aliyekuwa amemnunua.^d Alimtunza mwanakondoo huyo, naye akakua nyumbani mwake pamoja na wanawe. Mwanakondoo huyo alikuwa akila chakula kidogo alichokuwa nacho mtu huyo na kunywa kikombe chake, naye alikuwa akilala mikononi mwake. Mwanakondoo huyo akawa kama binti kwake. **4** Baadaye mgeni alimtembelea yule mwanamume tajiri, lakini mwanamume huyo hakutaka kuchukua mmoja wa kondoo wake mwenyewe au ng’ombe wake ili amchinjie msafiri aliyemtembelea. Badala yake alimchukua mwanakondoo wa yule mwanamume maskini na kumchinjia mgeni aliyemtembelea.”^e

5 Daudi aliposikia hayo, alikasirika sana kwa sababu ya mwanamume huyo, akamwambia Nathani: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi,^f mwanamume aliyefanya hivyo anastahili kufa! **6** Naye anapaswa kulipa mara nne zaidi kwa ajili ya mwanakondoo huyo,^g kwa sababu alifanya jambo hilo na hakuwa na huruma.”

7 Ndipo Nathani akamwambia Daudi: “Mwanamume huyo ni wewe! Yehova Mungu

wa Israeli anasema hivi: 'Mimi mwenyewe nilikutia mafuta uwe mfalme wa Israeli,^a nami nilikuokoa kutoka mikononi mwa Sauli.^b **8** Nilikuwa tayari kukupa nyumba ya bwana wako^c na kuwaweka mikononi mwako wake za^d bwana wako, nami nikakupa nyumba ya Israeli na ya Yuda.^e Na kana kwamba hayo hayatoshi, nilikuwa tayari kukufanyia mengi zaidi.^f **9** Kwa nini ulilidharau neno la Yehova, kwa kute nda lililo ovu machoni pake? Ulimuua Uria Mhiti kwa upanga!^g Kisha ukamchukua mke wake awe mke wako^h baada ya kumuua Uria kwa upanga wa Waamoni.ⁱ **10** Sasa upanga hautaondoka nyumbani mwako,^j kwa sababu ulinidharau kwa kumchukua mke wa Uria Mhiti awe mke wako.' **11** Yehova anasema hivi: 'Tazama, ninakuletea msiba kutoka katika nyumba yako mwenyewe;^k na mbele ya macho yako mwenyewe, nami nitawachukua wake zako na kumpa mwana mume mwingine,^l naye atalala na wake zako kweupe kabisa wakati wa mchana.*^m **12** Ingawa ulifanya jambo hilo kwa siri,ⁿ mimi nitafanya jambo hili mbele ya Waisraeli wote kweupe kabisa wakati wa mchana.'**^o

13 Ndipo Daudi akamwambia Nathani: "Nimemtendea Yehova dhambi."^p Nathani akamwambia Daudi: "Yehova naye amekusamehe dhambi uliyotenda.*^p Hutakufa.^q **14** Hata hivyo, kwa sababu hukumheshimu Yehova kamwe katika jambo hili, mwana wako aliye-

12:11, 12 *Au "juani." 12:13 *Au "amefutulia mbali dhambi yako."

SURA YA 12

a 1Sa 16:13
2Sa 7:8

b 1Sa 18:10, 11
1Sa 19:10
1Sa 23:14

c 1Sa 13:13, 14
1Sa 15:26, 28

d 2Sa 3:7
1Fa 2:22

e 2Sa 2:4
2Sa 5:5

f 2Sa 7:19

g Kut 20:13

h Kut 20:14, 17

i 2Sa 11:15, 27

j Hes 14:18
2Sa 13:32
2Sa 18:33
Gal 6:7

k 2Sa 12:15, 19
2Sa 13:10-15
2Sa 15:14

l Kut 21:24
Ayu 31:9-11
Ayu 34:11

m 2Sa 16:21, 22

n 2Sa 11:4, 15

o Mwa 39:9
Zb 32:5
Zb 38:3
Zb 51:Uta, 4
Met 28:13

p Kut 34:6
Zb 32:1

q Law 20:10
Zb 103:10

Safu ya 2

a 2Sa 12:22
Yon 3:8, 9

b Ru 3:3
2Sa 14:2

c 2Sa 6:17

zaliwa hivi punde, hakika atakufa."

15 Kisha Nathani akaenda nyumbani kwake.

Basi Yehova akamletea pigo mtoto ambaye mke wa Uria alikuwa amemzalia Daudi, akawa mgonjwa. **16** Daudi akamsihi sana Mungu wa kweli kwa ajili ya mvulana huyo. Daudi akafunga kabisa, naye alikuwa akiingia chumbani mwake na kulala chini usiku kucha.^a **17** Basi wazee wa nyumbani mwake wakasimama karibu naye na kujaribu kumwinua kutoka sakafuni, lakini alikataa, wala hakula pamoja nao. **18** Siku ya saba yule mtoto akafa, lakini watumishi wa Daudi wakaogopa kumwambia kwamba mtoto amekufa. Walisema: "Mtoto alipokuwa hai tulizungumza naye lakini hakutusikiliza. Sasa tutamwambiaje kwamba mtoto amekufa? Huenda akatenda jambo baya sana."

19 Daudi alipowaona watumishi wake wakinong'onezeana, alitambua kwamba yule mtoto amekufa. Daudi akawauliza: "Mtoto amekufa?" Wakajibu: "Amekufa." **20** Basi Daudi akainuka kutoka sakafuni. Akaoga, akajipaka mafuta,^b akabadili nguo zake, akaenda katika nyumba ya Yehova^c na kusujudu. Kisha akaenda nyumbani kwake* na kuomba aletewe chakula, naye akala. **21** Watumishi wake wakamuuliza: "Kwa nini umefanya hivi? Mtoto alipokuwa hai, ulifunga na kulia daima; lakini mara tu mtoto alipokufa ukainuka na kula chakula." **22** Akajibu:

12:20 *Au "katika jumba lake la mfalme."

"Mtoto alipokuwa hai, nilifunga^a na kulia daima kwa sababu nilisema moyoni, 'Ni nani ajuaye kama Yehova atanio-nyesha kibali na kumwacha mtoto aishi?'"^b **23** Sasa kwa kuwa amekufa, kwa nini nifunge? Je, naweza kumrudisha tena?^c Mimi nitamfuata,^d laki ni yeye hatanirudia mimi."^e

24 Kisha Daudi akamfariji Bath-sheba mke wake.^f Akaingia kwake na kulala naye. Baada ya muda akazaa mwana, akapewa jina Sulemani.^{*g} Yehova akampenda mwana huyo,^h **25** akamtuma nabii Nathaniⁱ amwite mtoto huyo Yedidia,^{*} kwa ajili ya Yehova.

26 Yoabu akaendelea kupigana na jiji la Raba^j la Waamoni,^k akaliteka jiji hilo la kifalme.^{*l} **27** Basi Yoabu akawatuma wajumbe kwa Daudi akisema: "Nimepigana na Raba,^m nami nimeliteka jiji lenye maji.^{*} **28** Sasa wakusanye wanajeshi waliobaki, upige kambi dhidi ya jiji hilo na kuliteka. La sivyo, mimi ndiye nitakayeliteka jiji hilo, na kusifiwa kwa kuliteka."^{*}

29 Basi Daudi akawakusanya wanajeshi wote na kwenenda Raba, akapigana nalo na kuliteka. **30** Kisha akachukua taji lililokuwa kwenye kichwa cha Malkamu. Uzito wa taji hilo ulikuwa talanta moja^{*} ya dhahabu, nalo lilikuwa na mawe yenye thamani, Daudi

12:24 *Jina hilo linatokana na neno la Kiebrania linalomaanisha "Amani." **12:25** *Maana yake "Mpendwa wa Yah." **12:26** *Au "jiji la ufalme huo." **12:27** *Huenda maneno haya yanarejelea vyanzo vya maji vya jiji hilo. **12:28** *Tnn., "nalo litaitwa kwa jina langu." **12:30** *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 12

a 2Sa 12:16
Yoe 1:14

b Isa 38:3, 5
Yoe 2:13, 14
Amo 5:15
Yon 3:8, 9

c Mhu 9:6

d Ayu 30:23
Mhu 3:20
Mdo 2:29, 34
Mdo 13:36

e Mhu 9:5, 10

f 2Sa 11:3

g 1Nya 3:5, 9
1Nya 22:9
1Nya 28:5
Mt 1:6

h 2Sa 7:12
1Nya 29:1

i 2Sa 7:4, 5
2Sa 12:1
1Fa 1:8

j Kum 3:11
Yos 13:24, 25

k Kum 23:3, 6

l 2Sa 11:25
1Nya 20:1

m 2Sa 11:1

Safu ya 2

a 2Sa 8:11, 12

b 1Nya 20:2, 3

SURA YA 13

c 1Nya 3:9

d 2Sa 3:2

e 2Sa 13:35

f 1Sa 16:9
1Nya 2:13

g Law 18:9
Law 20:17

akavishwa taji hilo kichwani. Alichukua pia nyara nyingi sana^a kutoka katika jiji hilo.^b **31** Akawatoa nje watu waliokuwa ndani yake, akawapa kazi ya kukata mawe kwa misumeno, vifaa vya chuma vyenye ncha kali na mashoka ya chuma, na kazi ya kufyatua matofali. Hivyo ndivyo alivyofanya katika majiji yote ya Waamoni. Hatimaye Daudi na wanajeshi wote wakarudi Yerusalemu.

13 Sasa Absalomu mwana wa Daudi alikuwa na dada mrembo aliyeitwa Tamari,^c basi Ammoni^d mwana wa Daudi akampenda. **2** Ammoni akateseka sana hivi kwamba akawa mgonjwa kwa sababu ya Tamari dada yake, kwa maana alikuwa bikira na ilionekana kwamba haiwezekani kwa Ammoni kumfanyia jambo lolote. **3** Sasa Ammoni alikuwa na rafiki aliyeitwa Yehonadabu,^e mwana wa Shimea,^f ndugu ya Daudi; na Yehonadabu alikuwa mtu mjanja sana. **4** Kwa hiyo akamuuliza: "Kwa nini wewe, mwana wa mfalme, unasononeka kila asubuhi? Kwa nini usiniambie?" Ammoni akamjibu hivi: "Ninampenda Tamari, dada^g ya ndugu yangu Absalomu." **5** Yehonadabu akamwambia: "Lala kিতandani mwako, ujifanye mgonjwa. Baba yako akija kukuona, mwambie, 'Tafadhali, mruhusu dada yangu Tamari aje kuniandalia chakula kidogo. Akitayarisha chakula cha mgonjwa^{*} mbele ya macho yangu nitakichukua kutoka mkononi mwake na kula.'" **13:5** *Au "mkate wa faraja."

6 Basi Amnoni akalala kitandani na kujifanya mgonjwa, hivyo mfalme akaja kumwona. Ndipo Amnoni akamwambia mfalme: "Tafadhali, mruhusu dada yangu Tamari aje kuniokea keki mbili zenye umbo la moyo mbele ya macho yangu, ili nichukue chakula kutoka mkononi mwake." **7** Kwa hiyo Daudi akamtumia Tamari ujumbe nyumbani, akisema: "Tafadhali, nenda katika nyumba ya ndugu yako Amnoni, umtayarishie chakula."* **8** Basi Tamari akaenda katika nyumba ya ndugu yake Amnoni, alimokuwa amelala. Akachukua unga, akaukanda na kuoka keki mbele ya Amnoni. **9** Kisha akachukua kikaango na kumpa keki hizo. Lakini Amnoni akakataa kula, akasema: "Waambie watu wote waondoke!" Basi watu wote waondoka.

10 Kisha Amnoni akamwambia Tamari: "Niletee chakula* katika chumba cha kulala, ili nikichukue kutoka mkononi mwako na kukila." Basi Tamari akachukua keki zenye umbo la moyo ambazo alikuwa ameoka na kumletea Amnoni ndugu yake katika chumba cha kulala. **11** Alipomletea ili ale, Amnoni akamkamata kwa nguvu na kumwambia: "Njoo, ulale nami, dada yangu." **12** Lakini Tamari akamwambia: "Usifanye hivyo ndugu yangu! Usiniaibishe, kwa maana jambo kama hili halipaswi kufanywa katika Israeli.^a Usitende jambo hili la aibu.^b **13** Nitaondoaje aibu yangu? Nawe utaoonwa kuwa kama mmojawapo wa wanau-

13:7 *Au "mkate wa faraja." 13:10 *Au "Niletee mkate wa faraja."

SURA YA 13

a Law 18:9, 29
Law 20:17
Kum 27:22

b Mwa 34:2, 7
Amu 20:5, 6

Safu ya 2

a Yos 7:6
Est 4:1
Yer 6:26

b 2Sa 3:3
2Sa 13:1

c Law 18:9
Kum 27:22

me wapumbavu katika Israeli. Sasa, tafadhali, ongea na mfalme, kwa maana hataku-kataza unichukue." **14** Lakini Amnoni akakataa kumsikiliza, akamzidi nguvu Tamari na kumwaibisha kwa kumba-ka. **15** Kisha Amnoni akainza kumchukua kwa chuki kali sana, hivi kwamba chuki hiyo ikawa kubwa sana kuliko upendo alikuwa nao mwanzoni kumwelekea. Amnoni akamwambia: "Inuka; nenda zako!" **16** Ndipo Tamari akamwambia: "Usinifukuze, ndugu yangu, kwa maana kitendo cha kunifukuza sasa ni kibaya zaidi kuliko jambo ulionitendea!" Lakini Amnoni akakataa kumsikiliza.

17 Basi akamwita kijana aliyemtumikia na kumwambia: "Tafadhali, mwondoe mtu huyu mbele yangu, na ufunge mlango." **18** (Sasa Tamari alikuwa amevaa joho la pekee,* kwa maana hayo ndiyo mavazi yaliyovaliwa na mabinti wa mfalme waliokuwa mabikira.) Kwa hiyo mtumishi huyo akamtoa nje na kufunga mlango. **19** Tamari akatia majivu kichwani mwake,^a akalirarua joho bora alilokuwa amevaa; akaweka mikonono yake kichwani na kwenenda zake, huku akilia kwa sauti alipokuwa akitembea.

20 Ndipo Absalomu ndugu yake^b akamuuliza: "Je, ni Amnoni ndugu yako aliyelala nawe? Sasa nyamaza, dada yangu. Yeye ni ndugu yako.^c Usiruhusu jambo hili likae moyoni mwako." Hivyo, Tamari akaishi peke yake katika nyumba ya Absalomu ndugu yake.

13:18 *Au "lenye mapambo."

21 Mfalme Daudi aliposikia mambo hayo yote, alikasirika sana.^a Lakini hakutaka kumuumiza hisia Amnoni mwana, kwa sababu alimpenda, na alikuwa mzaliwa wake wa kwanza. **22** Absalomu hakumwambia Amnoni jambo lolote jema au baya; kwa maana Absalomu alimchukia^b Amnoni kwa sababu alikuwa amewaibisha Tamari dada yake.^c

23 Baada ya miaka miwili kamili, wakataji manyoya ya kondoo wa Absalomu walipokuwa kule Baal-hasori, karibu na Efraimu,^d Absalomu aliwaalika wana wote wa mfalme.^e **24** Basi Absalomu akaja kwa mfalme na kumwambia: “Kondoo wangu, mimi mtumishi wako, wanakatwa manyoya. Nakuomba wewe mfalme na watumishi wako twnde pamoja.” **25** Lakini mfalme akamwambia Absalomu: “La, mwanangu. Tukienda sisi sote, tutakuwa mzigo kwako.” Ingawa aliendelea kumsihi, mfalme hakukubali kwenda, lakini alimbariki. **26** Ndipo Absalomu akamwambia: “Ikiwa hutaenda, tafadhali mruhusu Amnoni ndugu yangu aende pamoja nasi.”^f Mfalme akamuuliza: “Kwa nini aende pamoja nawe?” **27** Lakini Absalomu akamsihi, kwa hiyo mfalme akamruhusu Amnoni na wana wote wa mfalme waende pamoja na Absalomu.

28 Kisha Absalomu akawaagiza hivi watumishi wake: “Mwangelieni Amnoni, moyo wake utakapokuwa umechangamka kwa sababu ya divai, nitawaambia, ‘Mueni Amnoni!’ Ndipo mtakapomuua. Msiogope. Je, si mimi ndiye huwaamuru? Iweni imara

SURA YA 13

a Met 19:13

b Met 18:19

c Mwa 34:7

d Yoh 11:54

e 1Fa 1:9,19

f Zb 55:21
Met 10:18
Met 26:24-26

Safu ya 2

a 2Sa 13:3

b 1Sa 16:9
1Nya 2:13

c 2Sa 12:10

d Mwa 27:41
Zb 7:14
Met 18:19

e 2Sa 13:12-14

f Law 18:9, 29

g 2Sa 13:38

h 2Sa 13:3

na jasiri.” **29** Basi watumishi wa Absalomu wakamtendea Amnoni kama Absalomu alivyowaagiza; kisha wana wale wengine wa mfalme wakainuka, na kila mmoja wao akapanda nyumbu wake na kukimbia. **30** Walipokuwa njiani, habari hii ikamfikia Daudi: “Absalomu amewaua wana wote wa mfalme, na haku-na hata mmoja aliyebaki hai.” **31** Ndipo mfalme akasimama, akararua mavazi yake, na kulala chini, nao watumishi wake wote walikuwa wamesimama kando yake na mavazi yao yalikuwa yameraruliwa.

32 Hata hivyo, Yehonadabu^a mwana wa Shimea,^b ndugu ya Daudi, akasema: “Bwana wangu usifikiri kwamba wamewaua wana wote wa mfalme, kwa maana Amnoni peke yake ndiye aliyekufa.”^c Absalomu ndiye aliyeeagiza auawe kwa sababu alikuwa amekusudia kufanya hivyo^d tangu Amnoni alipomwai-bisha Tamari^e dada yake.^f **33** Sasa bwana wangu mfalme usisikilize habari hii inayosema, ‘Wana wote wa mfalme wamekufa’; ni Amnoni peke yake aliyekufa.”

34 Wakati huo, Absalomu akakimbia.^g Baadaye mlinzi akainua macho yake, akaona watu wengi wakija barabarani nyuma yake kando ya mlima. **35** Ndipo Yehonadabu^h akamwambia mfalme: “Tazama! Wana wa mfalme wamerudi, kama tu nilivyokwambia mimi mtumishi wako.” **36** Mara tu alipomaliza kuzungumza, wana wa mfalme wakaingia, wakilia kwa sauti; mfalme pia na watumishi wake wote wakalia kwa uchungu sana.

37 Lakini Absalomu akakimbia na kwenda kwa Talmái^a mwana wa Amihudi mfalme wa Geshuri. Daudi akamwombolezea mwana wake kwa siku nyingi. 38 Absalomu alipokimbia na kwenda Geshuri,^b alikaa huko kwa miaka mitatu.

39 Mwishowe Mfalme Daudi akatamani kwenda kumwona Absalomu, kwa maana alikuwa ametulia* baada ya kifo cha Amnoni.

14 Sasa Yoabu mwana wa Seruya^c akatambua kwamba moyo wa mfalme ulitamani kumwona Absalomu.^d 2 Kwa hiyo Yoabu akatuma watu huko Tekoa^e wamlete mwanamke mwerevu, akamwambia hivi: "Tafadhali, jifanye kana kwamba unao-mboleza, nawe uvae nguo za kuomboleza, na usijipake mafuta.^f Jifanye kama mwanamke ambaye amekuwa akio-mboleza kwa siku nyingi kwa sababu ya kufiwa. 3 Kisha uende kwa mfalme na kumwambia hivi." Basi Yoabu akamwambia mambo ya kusema.*

4 Mwanamke huyo Mtekoa akaenda kwa mfalme, akaanguka chini kifudufudi, akainama na kusema: "Ee mfalme, nisaidie!" 5 Mfalme akamuuliza: "Kuna shida gani?" Mwanamke huyo akasema: "Mimi ni mjane; mume wangu amekufa. 6 Nami, mtumishi wako, nilikuwa na wana wawili, nao wakapigana walipokuwa shambani. Hapakuwa na mtu wa kuwatangani-sha, mwana mmoja akampiga mwenzake na kumuua.

13:39 *Au "amepata faraja." 14:3 *Tnn., "akayatia maneno hayo kinywani mwake."

SURA YA 13

a 2Sa 3:3

b Kum 3:14
Yos 12:4, 5
2Sa 14:23

SURA YA 14

c 2Sa 2:18
1Nya 2:15, 16d 2Sa 13:39
2Sa 18:33
2Sa 19:2e 2Nya 11:5, 6
2Nya 20:20
Amo 1:1f Mhu 9:8
Da 10:3

Safu ya 2

a Hes 35:19
Kum 19:11, 12b Hes 35:19, 27
Kum 19:6c Kum 6:13
Mhu 8:4

7 Sasa watu wote wa familia wako dhidi yangu, mimi mtumishi wako, nao wanasema, 'Mtoe yule aliyemua ndugu yake, ili tumuue kwa sababu ya uhai wa* ndugu yake ambaye alimua,^a hata kama tutamwangamiza mrithi wake!' Watakuwa wamezima kaa langu la mwisho linalowaka,[#] na mume wangu hatakuwa na jina wala mzao^Δ duniani."

8 Ndipo mfalme akamwambia mwanamke huyo: "Nenda nyumbani kwako, nami nitatoa agizo kukuhusu."

9 Mwanamke huyo Mtekoa akamwambia mfalme: "Ee bwana wangu mfalme, hatia na iwe juu yangu na juu ya nyumba ya baba yangu, lakini wewe mfalme na kiti chako cha ufalme hakina hatia." 10 Mfalme akamwambia: "Mtu yeyote akizungumza nawe tena, mlete kwangu, naye hatakusumbua tena kamwe." 11 Lakini mwanamke huyo akasema: "Tafadhali mfalme, mkumbuke Yehova Mungu wako, ili mtu anayelipiza kisasi cha damu^b asilete maangamizi zaidi kwa kumuua mwanangu." Mfalme akasema: "Kwa hakika kama Yehova anavyoishi,^c hakuna hata unywele mmoja wa mwana wako utakaoanguka chini." 12 Ndipo mwanamke huyo akasema: "Tafadhali, niruhusu mimi mtumishi wako, ni kwambie neno moja, bwana wangu mfalme." Basi mfalme akasema: "Niambie!"

13 Mwanamke huyo akasema: "Kwa nini, basi, umefikiria kuwatendea watu wa Mu-

14:7 *Au "nafsi ya." #Yaani, tumaini la mwisho la kupata wazao. ΔTnn., "baki."

ngu jambo kama hilo?^a Mfalme akisema jambo kama hilo, anajitia katika hatia, kwa sababu mfalme hamrudishi mwana wake aliyefukuzwa.^b **14** Hakika tutakufa na kuwa kama maji yanayomwagwa chini, ambayo hayawezi kuzolewa. Lakini Mungu haondoi uhai,* naye hufikiria sababu za kumrudisha yule aliyefukuzwa. **15** Nimekuja kukwambia jambo hili bwana wangu mfalme kwa sababu watu walinitia woga. Basi mimi mtumishi wako nikasema, ‘Tafadhali, niruhusu nizingumze na mfalme. Huenda mfalme atatimiza ombi langu, mimi mtumwa wake. **16** Huenda mfalme akasikiliza na kuniokoa mimi mtumwa wake kutoka mikononi mwa mtu anayetaka kuniangamiza mimi na mwanangu wa pekee kutoka kwa urithi ambao Mungu alitupatia.’^c **17** Kisha mimi mtumishi wako nikasema, ‘Acha neno la bwana wangu mfalme linitulize,’ kwa maana bwana wangu mfalme ni kama malaika wa Mungu wa kweli katika kutofautisha jambo lililo jema na lililo baya. Yehova Mungu wako awe pamoja nawe.”

18 Basi mfalme akamwambia mwanamke huyo: “Tafadhali, usinifiche jambo lolote nitakalokuuliza.” Mwanamke huyo akamwambia: “Tafadhali, sema bwana wangu mfalme.” **19** Basi mfalme akamuuliza: “Je, Yoabu ndiye aliyekuambia ufanye hivi?”^d Mwanamke huyo akajibu: “Kwa hakika kama unavyoishi, Ee bwana wangu mfalme,

14:14 *Au “nafsi.”

SURA YA 14

a Kut 19:5
Hes 6:27

b 2Sa 13:38

c 2Sa 14:2,7

d 2Sa 14:1-3

Safu ya 2

a 2Sa 14:13

b 2Sa 13:38

c Kum 3:14
2Sa 3:3
2Sa 13:37

ni kama tu ulivyosema bwana wangu mfalme, kwa kuwa Yoabu mtumishi wako ndiye aliyeniagiza mimi mtumishi wako na kuniambia niseme maneno hayo yote.* **20** Mtumishi wako Yoabu amefanya hivyo ili mambo yaonekane tofauti, lakini wewe bwana wangu una hekima kama ya malaika wa Mungu wa kweli na unajua mambo yote yanayotendeka nchini.”

21 Basi mfalme akamwambia Yoabu: “Sawa, nitafanya jambo hilo.^a Nenda ukamlete kijana Absalom.”^b **22** Ndipo Yoabu akaanguka chini kifudufudi, akainama na kumsifu mfalme. Yoabu akasema: “Leo mimi mtumishi wako ninajua kwamba nimepata kibali machoni pako, Ee bwana wangu mfalme, kwa maana wewe mfalme umetimiza ombi langu, mimi mtumishi wako.” **23** Kisha Yoabu akaondoka kwenda Geshuri^c na kumleta Absalomu Yerusalemu. **24** Hata hivyo, mfalme akasema: “Acha arudi nyumbani kwake, lakini hatauona uso wangu.” Basi Absalomu akarudi nyumbani kwake, naye hakuuona uso wa mfalme.

25 Sasa katika Israeli yote, hakuna mwanamume yeyote aliyesifiwa kwa sura yake nzuri kama Absalomu. Hakuwa na kasoro yoyote, kuanzia wayo wa mguu mpaka utosi wa kichwa chake. **26** Aliponyoa kichwa chake—kwa maana alikinyoa mwishoni mwa kila mwaka kwa sababu nywele zake zilikuwa nzito sana—nywele hizo zilikuwa

14:19 *Tnn., “kutia maneno hayo yote katika kinywa changu.”

na uzito wa shekeli 200* kulingana na mizani ya kifalme.[#] **27** Absalomu alizaa wana watatu^a na binti mmoja ambaye aliitwa Tamari. Alikuwa mwanamke mrembo sana.

28 Absalomu akaendelea kuishi Yerusalemu kwa miaka miwili kamili, lakini hakuuona uso wa mfalme.^b **29** Basi Absalomu akamwita Yoabu ili amtume kwa mfalme, lakini Yoabu akakataa kuja. Kisha akatuma mtu amwite kwa mara ya pili, lakini bado akakataa kuja. **30** Mwishowe akawaambia watumishi wake: “Shamba la Yoabu liko kando ya shamba langu, nalo lina shayiri. Nendeni mkalichome moto.” Basi watumishi wa Absalomu wakalichoma moto shamba hilo. **31** Yoabu akaenda nyumbani kwa Absalomu na kumuuliza: “Kwa nini watumishi wako walilichoma moto shamba langu?” **32** Absalomu akamjibu Yoabu: “Tazama! nilikutumia ujumbe huu, ‘Njoo nikutume kwa mfalme, umuulize: “Kwa nini niliondoka Geshuri?^c Afadhali ninge-kaa huko. Sasa acha nikauone uso wa mfalme, na ikiwa nina hatia, basi anue.””

33 Kwa hiyo Yoabu akaenda kwa mfalme na kumwambia. Kisha akamwita Absalomu, naye akaja kwa mfalme na kuanguka chini kifudufudi, mbele ya mfalme. Kisha mfalme akambusu Absalomu.^d

14:26 *Karibu kilogramu 2.3. Angalia Nyongeza B14. [#]Huenda ilikuwa mizani yenye kipimo hususa iliyotumiwa katika jumba la mfalme au shekeli ya “kifalme” iliyokuwa tofauti na shekeli ya kawaida.

SURA YA 14

a 2Sa 18:18

b 2Sa 14:24

c 2Sa 14:23

d Mwa 45:15

Safu ya 2

SURA YA 15

a 1Sa 8:11

1Fa 1:5

Met 11:2

b Kum 25:7

Ru 4:1

c 1Sa 8:20

2Sa 8:15

d Zb 10:9

Zb 55:21

Met 26:25

e Met 11:9

f 2Sa 3:2

g 2Sa 13:38

2Sa 14:23

h Law 22:21

15 Baada ya mambo hayo yote, Absalomu akajipatia gari na farasi na watu 50 wa kukimbia mbele yake.^a **2** Absalomu alikuwa akiamka mapema na kusimama kando ya barabara iliyoelekea kwenye lango la jiji.^b Absalomu alikuwa akimwita na kumuuliza hivi mtu yeyote aliyekuwa na kesi ambayo ilipaswa kumuuliwa na mfalme:^c “Unatoka jiji gani?” naye alijibu: “Mimi mtumishi wako ninatoka katika mojawapo ya makabila ya Waisraeli.” **3** Kisha Absalomu alimwambia: “Madai yako ni ya kweli na ya haki, lakini hakuna yeyote kutoka kwa mfalme wa kusikiliza kesi yako.” **4** Absalomu alimwambia: “Laiti ningewekwa kuwa mwamuzi nchini! Kila mtu aliyena na kesi au mashtaka angekuja kwangu, nami ningehakikisha kwamba anatendewa haki.”

5 Mtu alipomkaribia ili amwinamie, Absalomu alikuwa akinyoosha mkono wake na kumshika na kumbusu.^d **6** Absalomu alikuwa akiwafanyia hivyo Waisraeli wote waliokuwa wakienda kwa mfalme kuwasilisha mashtaka yao; basi Absalomu akaendelea kuiba moyo ya Waisraeli.^e

7 Mwishoni mwa miaka minne,^{*} Absalomu akamwambia mfalme: “Tafadhali, acha niende Hebroni^f nikatimize nadhiri yangu niliyomwekea Yehova. **8** Kwa maana mimi mtumishi wako nilipokuwa ni-kiishi Geshuri^g huko Siria niliweka nadhiri hii takatifu:^h ‘Ikiwa Yehova atanirudisha Yerusalemu, nitamtotea Yeho-

15:7 *Au labda, “miaka 40.”

va dhabihu.”* **9** Basi mfalme akamwambia: “Nenda kwa amani.” Absalomu akaondoka na kwenda Hebroni.

10 Sasa Absalomu akawatumia wapelelezi katika makabila yote ya Israeli, akawaambia: “Mara tu mtakaposisikia sauti ya pembe, tanga-zeni hivi: ‘Absalomu amekuwa mfalme katika Hebroni!’”^a

11 Absalomu alikuwa amee-nda huko na wanaume 200 kutoka Yerusalemu; alikuwa amewakaribisha, nao hawakushuku wala kujua kilichokuwa kikiendelea. **12** Isitoshе, Absalomu alipotoa dhabihu, aliwatuma watu wamwite Ahithofeli^b Mgiloni, mshauri wa Daudi,^c kutoka jiji la Gilo.^d Njama iliendelea kupamba moto, na idadi ya watu waliomuunga mkono Absalomu ikaendelea kuongezeka.^e

13 Baada ya muda mpelelezi fulani akaja kwa Daudi na kumwambia: “Mioyo ya watu wa Israeli imegeuka kumfuata Absalomu.” **14** Mara moja Daudi akawaambia watumishi wake wote waliokuwa pamoja naye huko Yerusalemu: “Tuondoke, tukimbie,^f kwa maana hakuna yeyote kati yetu atakayemkwepa Absalomu! Fanyeni haraka, asiye akatufikia na kutuletea msiba na kuwaua watu wote jijini kwa upanga!”^g **15** Watumishi wa mfalme wakamwambia mfalme: “Lolote ambalo wewe bwana wetu mfalme utaamua, sisi watumishi wako tuko tayari kulifanya.”^h **16** Basi mfalme akatoka pamoja na watu wote wa nyumbani mwake, lakini mfalme akawaa-

15:8 *Au “nitamwabudu; nitamtumikia.”

SURA YA 15

a 2Sa 2:1
2Sa 5:1, 5
1Nya 3:4

b 2Sa 16:23
2Sa 17:14
2Sa 23:8, 34

c Zb 41:9
Zb 55:12, 13
Yoh 13:18

d Yos 15:20, 51

e Zb 3:1
Met 24:21

f 2Sa 19:9
Zb 3:Uta

g 2Sa 12:11

h Met 18:24

Safu ya 2

a 2Sa 12:11
2Sa 16:21
2Sa 20:3

b 2Sa 8:18
2Sa 20:7
1Fa 1:38
1Nya 18:17

c Yos 13:2, 3

d 1Sa 27:4
1Nya 18:1

e 2Sa 18:2

f 2Sa 2:5, 6
Zb 25:10
Zb 57:3
Zb 61:7
Zb 89:14

g Met 17:17
Met 18:24

h 2Sa 18:2

cha masuria kumi^a ili watunze nyumba.* **17** Mfalme akaondoka pamoja na watu wote waliokuwa pamoja naye, wakasimama Beth-merhaki.

18 Watumishi wake wote walioondoka pamoja naye* na Wakerethi wote na Wapelethi^b wote na Wagathi^c wote, watu 600 waliokuwa wamemfuata kutoka Gathi,^d wakapita mbele yake akiwachunguza.^e **19** Ndipo mfalme akamwambia Itai^e Mgathi: “Kwa nini wewe pia uende pamoja nasi? Rudi ukaishi na mfalme mpya, kwa sababu wewe ni mgeni, na pia ulifukuzwa kutoka katika nchi yako.

20 Ulikuja jana tu, kwa nini leo nikufanye utange-tange pamoja nasi, uende wakati ninapohitaji kwenda na mahali popote ninapoenda? Rudi pamoja na ndugu zako, na Yehova akutendee kwa upendo mshikamanifu na kwa uaminifu!”^f **21** Lakini Itai akamwambia mfalme: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kwa hakika kama bwana wangu mfalme anavyoishi, mahali popote utakapokuwa wewe bwana wangu mfalme, ukiwa hai au ukiwa umekufa, mimi mtumishi wako nitakuwa mahali hapo!”^g **22** Ndipo Daudi akamwambia Itai:^h “Pita uvuke.” Basi Itai Mgathi akavuka, pamoja na watu wake wote na watoto wake.

23 Watu wote nchini wali-kuwa wakilia kwa sauti ku-bwa watu hao wote walipokuwa wakivuka ng’ambo ile nyingine, naye mfalme alikuwa amesimama kando ya Bonde

15:16 *Au “jumba la mfalme.”

15:18 *Au “waliovuka upande wake.” #Au “wakavuka mbele ya uso wa mfalme.”

la Kidroni;^a watu wote walivuka na kufuata barabara inayoelekea nyikani. **24** Sadoki^b pia alikuwa mahali hapo pamoja na Walawi wote^c waliobeba sanduku^d la agano la Mungu wa kweli;^e nao wakaliweka chini Sanduku la Mungu wa kweli; Abiathari^f pia alikuwepo watu wote walipovuka kutoka jijini. **25** Lakini mfalme akamwambia Sadoki: “Lirudishe jijini Sanduku la Mungu wa kweli.^g Nikipata kibali machoni pa Yehova, atanirudisha na kuniruhusu kuliona na kuona mahali linapokaa.^h **26** Lakini akisema, ‘Sipe ndezwi nawe,’ basi na anite ndee jambo lolote analoona ni jema.” **27** Mfalme akamwambia kuhani Sadoki: “Je, wewe si mwonaji?ⁱ Rudi jijini kwa amani, na pia wachukue wana wenu wawili, Ahimaazi mwana wako na Yonathani^j mwana wa Abiathari. **28** Nitangojea kando ya vivuko vya nyikani mpaka nitakapotea habari kutoka kwenu.”^k **29** Basi Sadoki na Abiathari wakalirudisha Sanduku la Mungu wa kweli Yerusalemu, nao wakabaki huko.

30 Daudi alipanda Mlima wa Mizeituni^l huku akilia; alikuwa amefunika kichwa chake, na alikuwa miguu mitupu. Pia watu wote waliokuwa pamoja naye walifunika vichwa vyao, nao walikuwa wakilia huku wakipanda. **31** Kisha Daudi akaambiwa hivi: “Ahithofeli ni miongoni mwa watu wanaopanga njama^m pamoja na Absalom.”ⁿ Daudi akasema: “Ee Yehova,^o tafadhali badili ushauri wa Ahithofeli uwe upumbavu!”^p

SURA YA 15

a 1Fa 2:36, 37
2Nya 30:14
Yoh 18:1

b 2Sa 8:17
2Sa 20:25
1Fa 1:8
1Fa 2:35
1Nya 6:8

c Hes 8:19

d Kut 37:1
Law 16:2

e Hes 4:15
Hes 7:9
1Nya 15:2

f 1Sa 22:20
1Sa 30:7

g 2Sa 6:17

h 2Sa 7:2
Zb 26:8
Zb 27:4

i 1Sa 9:9

j 2Sa 17:17

k 2Sa 15:36
2Sa 17:16, 21

l Mt 21:1
Mt 24:3
Mdo 1:12

m Zb 41:9
Zb 55:12, 13
Yoh 13:18

n Zb 3:Uta

o Zb 3:7

p 2Sa 16:23
2Sa 17:14

Safu ya 2

a 2Sa 16:16

b Yos 16:1, 2

c 2Sa 16:18, 19

d 2Sa 17:7, 14

e 2Sa 17:15, 16

f 2Sa 18:19

g 2Sa 17:17
1Fa 1:42

h 2Sa 16:16
1Nya 27:33

SURA YA 16

i 2Sa 15:30

j 2Sa 9:2, 9

k 2Sa 9:6

l 1Sa 25:18

32 Daudi alipofika kwenye kilele, mahali ambapo watu walizoea kumwinamia Mungu, Hushai^a Mwarki^b alikuwa mahali hapo ili kumpokea, joho lake lilikuwa limeraruka na alikuwa na mavumbi kichwani. **33** Hata hivyo, Daudi akamwambia: “Ukivuka kwenda pamoja nami, utakuwa mzigo kwangu. **34** Lakini ukirudi jijini nawe umwambie Absalom, ‘Mimi ni mtumishi wako, Ee mfalme. Nilikuwa mtumishi wa baba yako zamani, lakini sasa mimi ni mtumishi wako,’^c ndipo utakapoinisaidia kuvuruga ushauri wa Ahithofeli.^d **35** Kuhani Sadoki na Abiathari wako huko pamoja nawe. Utamwambia kuhani Sadoki na Abiathari mambo yote utakayosikia katika nyumba ya mfalme.^e **36** Wana wao wawili, Ahimaazi^f mwana wa Sadoki na Yonathani^g mwana wa Abiathari wako huko pamoja nao, nanyi mtawatumia wana hao kuniletea habari zote mtakazosikia.” **37** Basi Hushai rafiki ya^{*h} Daudi akaingia jijini Absalom alipokuwa akiingia Yerusalemu.

16 Daudi alipokuwa amepita mbele kidogo ya kilele,ⁱ Siba^j mtumishi wa Mefiboshethi^k alikuwa hapo ili kumpokea; alikuwa na punda wawili wenye matandiko, na walikuwa wamebeba mikate 200, keki 100 za zabibu kavu, keki 100 za matunda ya kiangazi,^{*} na mtungi mkubwa wa divai.^l **2** Mfalme akamuuliza Siba: “Kwa nini umeleta vitu hivi?” Siba aka-

15:37 *Au “msiri wa.” **16:1** *Hasa tini na labda pia tende.

mjibu: "Punda ni kwa ajili ya nyumba ya mfalme ili wapande juu yao, mikate na matunda ya kiangazi ni kwa ajili ya vijana, na divai ni kwa ajili ya wale watakaochoka nyikani."^a **3** Mfalme akamuuliza: "Na mwana wa bwana wako yuko wapi?"^b Siba akamwambia mfalme: "Yuko Yerusalemu, kwa maana alisema, 'Leo nyumba ya Israeli itanirudishia utawala wa kifalme wa baba yangu.'"^c **4** Ndipo mfalme akamwambia Siba: "Tazama! Mali yote ya Mefiboshethi ni yako."^d Siba akasema: "Nainama mbele yako. Acha nipa-te kibali machoni pako, bwana wangu mfalme."^e

5 Mfalme Daudi alipofika Bahurimu, mtu fulani kuto-ka katika ukoo wa nyumba ya Sauli anayelitwa Shimei,^f mwana wa Gera, akaja kumtukana Daudi huku akimkaribia.^g **6** Alikuwa akimtu-pia Daudi mawe, na watumishi wote wa Mfalme Daudi, pamo-ja na watu wote na wanaume mashujaa waliokuwa upande wake wa kulia na wa kushoto. **7** Shimei alimtukana aki-sema: "Ondoka, ondoka, wewe mtu mwenye hatia ya damu! Wewe mtu asiyefaa kitu!" **8** Yehova amekulipiza kwa sa-babu ya hatia yote uliyopata kwa kumwaga damu ya watu wa nyumba ya Sauli, ambaye umechukua mahali pake na kutawala ukiwa mfalme, laki-ni Yehova anautia ufalme mi-kononi mwa Absalomu mwa-na wako. Sasa msiba umeku-pata kwa sababu wewe ni mtu mwenye hatia ya damu!"^h

9 Ndipo Abishai mwana wa Seruyaⁱ akamwambia mfalme: "Kwa nini huyu mbwa mfu-

SURA YA 16

a 2Sa 17:27-29

b 2Sa 9:3

c 2Sa 19:25-27

d 2Sa 9:9,10

e Met 26:22

f 2Sa 19:16
1Fa 2:8,44

g Kut 22:28
Mhu 10:20

h 1Sa 24:6,7
1Sa 26:9,11
Zb 3:1,2
Zb 7:1
Zb 71:10,11

i 1Nya 2:15,16

j 1Sa 24:14

Safu ya 2

a Kut 22:28

b 1Sa 26:8

c 2Sa 19:22
1Fa 2:5

d Zb 37:8
1Pe 2:23

e 2Sa 12:10

f 2Sa 12:11
2Sa 15:14
2Sa 17:12

g 2Sa 19:16

h Mwa 29:32
Kut 3:7
Zb 25:18

i Zb 109:28

j 2Sa 16:5

k 2Sa 15:12,31

l 2Sa 15:32,37
1Nya 27:33

m Yos 16:1,2

n 1Fa 1:25

akutukane bwana wangu mfalme?"^a Tafadhali niruhusu nivuke, nikamkate kichwa."^b

10 Lakini mfalme akasema: "Nina nini nanyi, enyi wana wa Seruya?"^c Mwacheni anitukane,^d kwa sababu Yehova amemwambia,^e 'Mtukane Daudi!' Basi ni nani anayepaswa kumuuliza, 'Kwa nini unafanya hivi?' **11** Kisha Daudi akamwambia Abishai na watumishi wake wote: "Ikiwa mwangu mwenyewe, niliyemzaa anatafuta uhai wangu,^f je, Mbenjamini hatafanya zaidi?"^g Mwacheni anitukane, kwa maana Yehova alimwambia afanye hivyo! **12** Huenda Yehova ataona mateso yangu,^h na Yehova atanilipa kwa wema badala ya matusi niliyotukanwa leo hii."ⁱ **13** Kwa hivyo Daudi na wanaume wake wakaendelea kuteremka barabarani huku Shimei akitembea kando ya mlima sambamba na Daudi, naye alikuwa akimtukana kwa sauti,^j akitupa mawe na kurusha mavumbi mengi.

14 Hatimaye mfalme na watu wote waliokuwa pamoja naye wakafika wakiwa wamechoka mahali walikokuwa wakienda, nao wapakumzika.*

15 Wakati huo, Absalomu na wanaume wote wa Israeli wakafika Yerusalemu, na Ahithofeli^k alikuwa pamoja naye. **16** Hushai^l Mwariki,^m rafiki ya* Daudi, alipoingia kwa Absalomu, alimwambia hivi Absalomu: "Mfalme na aishi muda mrefu!"ⁿ Mfalme na aishi muda mrefu!" **17** Ndipo Absalomu akamuuliza Hushai:

16:11 *Au "nafsi yangu." 16:14 *Tnn., "wakajiburudisha." 16:16 *Au "msiri wa."

“Je, huu ndio upendo mshikamanifu unaomtendea rafiki yako? Kwa nini hukwenda na rafiki yako?” **18** Basi Hushai akamwambia Absalomu: “Siwezi kufanya hivyo, ninamuunga mkono yule aliyechaguliwa na Yehova, na watu hawa, na wanaume wote wa Israeli. Nitakaa pamoja naye. **19** Na kwa mara nyingine nasema, Ninapaswa kumtumikia nani? Je, sipaswi kumtumikia mwana wake? Kama nilivyomtumikia baba yako, ndivyo nitakavyokutumikia.”^a

20 Ndipo Absalomu akamwambia Ahithofeli: “Nipe ushauri.^b Tufanye nini?” **21** Basi Ahithofeli akamwambia Absalomu: “Fanya ngono na masuria wa baba yako,^c aliowaacha waitunze nyumba.*^d Kisha Waisraeli wote watasikia kwamba umekuwa uvundo kwa baba yako, na wale wanaokuunga mkono watapata nguvu.” **22** Kwa hiyo wakampigia hema Absalomu juu ya paa,^e naye Absalomu akafanya ngono na masuria wa baba yake^f Waisraeli wote wakitazama.^g

23 Siku hizo, ushauri uliotolewa na Ahithofeli^h ulionwa kama neno la* Mungu wa kweli. Hivyo ndivyo ushauri wote wa Ahithofeli ulivyothaminiwa, na Daudi na pia Absalomu.

17 Kisha Ahithofeli akamwambia Absalomu: “Tafadhali, niruhusu nichague wanaume 12,000 niende kumfuatia Daudi usiku wa leo. **2** Nitamkuta akiwa amechoka

16:21 *Au “walitunze jumba la mfalme.”

16:23 *Au “ulionwa kama ushauri uliotafutwa kutoka kwa.”

SURA YA 16

a 2Sa 15:34

b Zb 37:12

c Law 18:8
Law 20:11
1Fa 2:22

d 2Sa 15:16

e 2Sa 11:2

f Kum 22:30
2Sa 20:3

g 2Sa 12:11, 12

h 2Sa 15:12
2Sa 17:14, 23

Safu ya 2

SURA YA 17

a 2Sa 16:14

b Zb 37:12
Zb 41:9
Zb 55:12, 13c 2Sa 15:32
2Sa 16:16

d 2Sa 15:34

e 1Sa 16:18
2Sa 15:18
2Sa 23:8, 18
1Nya 11:26

f Met 17:12

g 1Sa 17:50
1Sa 18:7
1Sa 19:8
2Sa 10:18h 1Sa 22:1
1Sa 23:19i Mwa 49:9
2Sa 1:23
1Sa 31:4

na akiwa dhaifu,^{*a} kisha nita mtia woga; na watu wote walio pamoja naye watakimbia, nami nitamuua mfalme peke yake.^b **3** Halafu nitawarudisha watu wote kwako. Kurudi kwa watu wote kunategemea kitakachompata mtu unayemtafuta. Kisha watu wote watakuwa na amani.” **4** Pendekezo hilo lilikuwa zuri kabisa machoni pa Absalomu na wazee wote wa Israeli.

5 Hata hivyo, Absalomu akasema: “Tafadhali, mwite ni pia Hushai^c Mwarki, tusikie jambo atakalosema.” **6** Basi Hushai akaja kwa Absalomu. Kisha Absalomu akamwambia: “Huu ndio ushauri uliotolewa na Ahithofeli. Je, tufuate ushauri wake? Kama sivyo, tuambie jambo la kufanya.” **7** Ndipo Hushai akamwambia Absalomu: “Wakati huu, ushauri uliotolewa na Ahithofeli si mzuri!”^d

8 Hushai akaendelea kusema: “Unajua viziri kwamba baba yako na wanaume wake ni mashujaa,^e na wana hasira* kama dubu aliyepoteza watoto wake porini.^f Isitoshe, baba yako ni mpiganaji hodari,^g naye hatakaa usiku kucha na watu. **9** Sasa hivi amejificha ndani ya mojawapo ya mapango* au mahali pengine;^h ikiwa atakuwa wa kwanza kutushambulia, wale watakosikia habari hiyo watasema, ‘Watu wanaomfuata Absalomu wameshindwa!’ **10** Hata mwanaume jasiri aliye na moyo kama wa simbaⁱ hakika atanyong’onyea kwa woga, kwa maana Waisraeli wote wana-

17:2 *Au “amedhoofika mikono yote mwili.” 17:8 *Au “na wana uchungu nafsi.” 17:9 *Au “mashimo; mabonde.”

jua kwamba baba yako ni mwanamume shujaa^a na kwamba wanaume walio pamoja naye ni jasiri. **11** Natoa ushauri huu: Waisraeli wote na wakusanyike kwako, kuanzia Dani mpaka Beer-sheba,^b wengi kama chembe za mchanga kwenye ufuo wa bahari,^c nawe uwaongoze vitani. **12** Tutamshambulia mahali popote atakapopatikana, nasi tutamwangukia kama umande unavyoanguka ardhini; na hakuna hata mmoja wao atakayeokoka, wala yeye wala mwanamume yeyote aliye pamoja naye. **13** Ikiwa atakimbilia jiji fulani, Waisraeli wote watachukua kamba na kwenda katika jiji hilo na kuliburu-ta mpaka bondeni, na hakuna hata jiwe dogo litakalobaki.”

14 Ndipo Absalomu na wanaume wote wa Israeli wakasema: “Ushauri wa Hushai Mwarki ni bora^d kuliko ushauri wa Ahithofeli!” Kwa maana Yehova alikuwa amezimia* kuvuruga ushauri mzuri wa Ahithofeli,^e ili Yehova amletee msiba Absalomu.^f

15 Baadaye Hushai akamwambia Sadoki na Abiathari^g waliokuwa makuhani: “Hivi ndivyo Ahithofeli alivyomshauri Absalomu na wazee wa Israeli, na hivi ndivyo nilivyowashauri. **16** Sasa tumeni ujumbe haraka kwa Daudi na kumwonya hivi: ‘Usikae kwenye vivuko vilivyo nyikani usiku wa leo, lakini hakikisha umevuka, usipofanya hivyo, wewe mfalme na watu wote walio pamoja nawe mtaangamizwa.’”^h

17:14 *Au “amekusudia.” 17:16 *Tnn., “mtamezwa.”

SURA YA 17

a 1Sa 18:5

b Amu 20:1

c 1Fa 4:20

d Met 21:1

e 2Sa 15:31, 34
2Sa 16:23
Met 19:21
Met 21:30

f Kum 2:30
2Nya 25:20

g 2Sa 8:17
2Sa 15:35

h Zb 35:24, 25

Safu ya 2

a 1Fa 1:42

b 2Sa 15:27, 36
2Sa 18:19

c Yos 15:7, 12
Yos 18:16, 20
1Fa 1:9

d 2Sa 16:5
2Sa 19:16

e Kut 1:19
Yos 2:3-5
1Sa 19:12, 14
1Sa 21:2

f 2Sa 17:1, 2

17 Yonathani^a na Ahimaa-zi^b walikuwa wakikaa Enrogeli;^c basi kijakazi fulani akaenda na kuwaambia, nao wakaenda kumwambia Mfalme Daudi kwa maana hawakutaka kujihatarisha kwa kuonekana wakiingia jijini. **18** Hata hivyo, kijana fulani akawaona na kumwambia Absalomu. Basi wote wawili wakaondoka haraka na kwenda mpaka kwenye nyumba ya mtu fulani huko Bahurimu^d aliyekuwa na kisima katika ua wa nyumba yake. Wakaingia kisimani, **19** kisha mke wa mwanamume huyo akakifunika kisima hicho na kuweka chengachenga za nafaka juu yake; hakuna aliyejua jambo hilo. **20** Watumishi wa Absalomu wakaja kwa mwanamke huyo nyumbani kwake na kumuuliza: “Ahimaaazi na Yonathani wako wapi?” Mwanamke huyo akawajibu: “Walipita hapa wakanda kwenye maji.”^e Kisha wanaume hao wakawatafuta lakini hawakuwapata, basi wakarudi Yerusalemu.

21 Baada ya wanaume hao kwenda zao, walitoka kisimani na kwenda kumjulisha Mfalme Daudi. Wakamwambia: “Ondoka, uvuke haraka maji haya, kwa maana Ahithofeli ametoa ushauri dhidi yako.”^f **22** Mara moja Daudi na watu wote waliokuwa pamoja naye wakaondoka na kuvuka Yordani. Wakati wa mapambazuko, hapakuwa na mtu hata mmoja ambaye hakuwa amevuka Yordani.

23 Ahithofeli alipoona kwamba ushauri wake hauku-fuatwa, aliweka matandiko juu ya punda wake na kwenda

nyumbani kwake katika mji wao.^a Baada ya kuwapa maagizo watu wa nyumbani mwake,^b akajitia kitanzi.*^c Basi akafa na kuzikwa katika makaburi ya mababu zake.

24 Wakati huo, Daudi akaenda Mahanaimu,^d naye Absalomu akavuka Yordani pamoja na wanaume wote wa Israeli.

25 Absalomu alimweka Amasa^e kuwa msimamizi wa jeshi badala ya Yoabu;^f Amasa alikuwa mwana wa mwanamume Mwisraeli aliyelitwa Ithra, aliyelala na Abigaili,^g binti ya Nahashi, dada ya Seruya, mama ya Yoabu. **26** Waisraeli na Absalomu wakapiga kambi katika nchi ya Gileadi.^h

27 Mara tu Daudi alipofika Mahanaimu, Shobi mwana wa Nahashi kutoka katika jiji la Rabaⁱ la Waamoni, Makiri^j mwana wa Amieli kutoka Lodebari, na Barzilai^k Mgileadi kutoka Rogelimu **28** wakalita vitanda, mabeseni, vyungu, ngano, shayiri, unga, nafaka iliyokaangwa, maharagwe mapana, dengu, nafaka iliyokauka, **29** asali, siagi, kondoo, na jibini. Walimletea vitu hivyo vyote Daudi na watu waliokuwa pamoja naye ili wale,^l kwa maana walisema: "Watu wana njaa, wamechoka, na wana kiu nyikani."^m

18 Kisha Daudi akawahe-sabu watu waliokuwa pamoja naye na kuweka juu yao wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia.ⁿ **2** Na Daudi akatuma theluthi ya wanaume chini ya amri ya* Yoabu,^o na theluthi nyingine chini ya amri ya Abishai^p mwana

SURA YA 17

a Yos 15:20, 51
2Sa 15:12

b 2Fa 20:1

c 1Sa 31:4
1Fa 16:18
Zb 5:10
Zb 55:23
Mt 27:3, 5
Mdo 1:18

d Mwa 32:1, 2
Yos 13:24, 26

e 2Sa 19:13
2Sa 20:4, 10

f 2Sa 8:16

g 1Nya 2:16, 17

h Hes 32:1
Kum 3:15

i Kum 3:11
Yos 13:24, 25
2Sa 12:26, 29

j 2Sa 9:3-5

k 2Sa 19:31, 32
1Fa 2:7

l Met 11:25

m 1Sa 25:18
2Sa 16:2

SURA YA 18

n Met 20:18

o 2Sa 8:16
2Sa 10:7

p 2Sa 23:18, 19

Safu ya 2

a 1Nya 2:15, 16

b 2Sa 15:19, 21

c 2Sa 21:17

d 2Sa 17:1-3
Omb 4:20

e 2Sa 18:12

f 2Sa 17:26

g 2Sa 16:15

h Zb 3:7
Met 24:21, 22

wa Seruya,^a ndugu ya Yoabu, na theluthi nyingine chini ya amri ya Itai^b Mgathi. Kisha mfalme akawaambia wanaume hao: "Mimi pia nitaenda pamoja nanyi." **3** Lakini wakasema: "Usiende,^c kwa maana tukikimbia, hawatashughulika nasi;* na nusu yetu tukifa, hawatajali juu yetu, kwa maana thamani yako ni sawa na watu 10,000 miongoni mwetu.^d Kwa hiyo, litakuwa jambo bora zaidi ikiwa utatutumia msaada kutoka jijini."

4 Mfalme akawaambia: "Nita-fanya jambo lolote mnaloona ni jema zaidi." Kwa hiyo mfalme akasimama karibu na lango la jiji na wanaume wote wakatoka wakiwa katika makundi ya mamia na maelfu. **5** Kisha mfalme akampa agizo hili Yoabu, Abishai, na Itai: "Mtendeeni kwa upole kijana Absalomu kwa ajili yangu."^e Wanaume wote walimsikia mfalme akiwapa wakuu wote agizo hilo kuhusu Absalomu.

6 Wanaume hao wakaenda kupigana na Waisraeli, wali-pigana vita hivyo katika mtsitu wa Efraimu.^f **7** Huko, watu wa Israeli^g wakashindwa na watumishi wa Daudi,^h na wanaume wengi waka-uawa siku hiyo—wanaume 20,000. **8** Vita vikaenea katika eneo lote. Isitoshe, msitu uliwaua* watu wengi zaidi kuliko walioauwa kwa upanga siku hiyo.

9 Mwishowe Absalomu akatuna kwa ghafla na watumishi wa Daudi. Absalomu alikuwa amepanda juu ya nyumbu, na nyumbu huyo akaingia chi-

17:23 *Au "akajinyonga." 18:2 *Tnn., "mkono wa."

18:3 *Tnn., "hawataweka moyo wao juu yetu." 18:8 *Tnn., "uliwala."

ni ya matawi yaliyosongama-na ya mti mkubwa, na kichwa chake kikakwama kwenye mti huo hivi kwamba akabaki amening'inia hewani huku nyumbu wake akiendelea kukimbia. **10** Mtu fulani aliona jambo hilo na kumwambia Yoabu:^a "Jamani! Nimemwona Absalomu aking'inia kwenye mti mkubwa." **11** Yoabu akamwambia hivi mtu huyo: "Ikiwa ulimwona, kwa nini hukumuua papo hapo na kumwangusha chini? Ikiwa ungefanya hivyo, ningefuraha kukupa vipande kumi vya fedha na mshipi." **12** Lakini mtu huyo akamwambia Yoabu: "Hata kama ningepewa vipande 1,000 vya fedha, nisingeunyoosha mkono wangu dhidi ya mwana wa mfalme, kwa maana tulimsikia mfalme akikupa agizo hili, wewe na Abishai na Itai: 'Haidhuru wewe ni nani, mlindeni kijana Absalomu.'^b **13** Nisingetii na hivyo kumuua,* jambo hilo lingejulikana kwa mfalme siku moja, nawe hungenilinda." **14** Ndipo Yoabu akasema: "Sitaendelea kupoteza muda pamoja nawe!" Basi akachukua mikuki mitatu midogo* na kumchoma nayo Absalomu kwenye moyo alipokuwa angali hai aking'inia kwenye mti mkubwa. **15** Kisha watumishi kumi waliombebea Yoabu silaha wakaja na kumpiga Absalomu mpaka wakamuua.^c **16** Sasa Yoabu akapiga pembe, na watu wakarudi na kuacha kuwafuatia Waisraeli; Yoabu akawaambia wasiwafuatie. **17** Wakamchukua

18:13 *Au "Ikiwa ningeitendea nafsi yake kwa hila." **18:14** *Au labda, "vishale." Tnn., "fito za chuma."

SURA YA 18

a 2Sa 8:16
2Sa 18:2

b 2Sa 18:5

c 2Sa 12:10
Met 2:22
Met 20:20
Met 30:17

Safu ya 2

a Yos 7:24, 26
Yos 8:29
Yos 10:23, 27

b Mwa 14:17

c 2Sa 14:27

d 2Sa 15:35, 36
2Sa 17:17

e Zb 9:4

f 2Sa 18:5

g Mwa 10:6

Absalomu na kumtupa ndani ya shimo kubwa msituni, nao wakarundika rundo kubwa sana la mawe juu yake.^a Kisha Waisraeli wote wakakimbia na kurudi katika nyumba zao.

18 Absalomu alipokuwa hai, alikuwa amechukua na kujisimamishia nguzo katika Bonde la* Mfalme,^b kwa maana alisema: "Sina mwana atakayeendelea kumbukumbu ya jina langu."^c Basi akaiita nguzo hiyo kwa jina lake, na tangu siku hiyo inaitwa Mnara wa Ukumbusho wa Absalomu.

19 Ahimaazi^d mwana wa Sadoki akasema: "Tafadhali, niruhusu nikimbie na kumpelekea mfalme habari hizi, kwa maana Yehova amemtendea kwa haki kwa kumweka huru kutoka mikononi mwa maa-
dui wake."^e **20** Lakini Yoabu akamwambia: "Hutapeleka habari hizi leo. Unaweza kuzipeleka siku nyingine, lakini hutampeleka mfalme habari hizi leo kwa sababu aliyekufa ni mwana wake mwenyewe."^f

21 Kisha Yoabu akamwambia mtu fulani Mkushi:^g "Nenda, umwambie mfalme mambo uliyoona." Kwa hiyo Mkushi huyo akamwinamia Yoabu na kukimbia. **22** Ahimaazi mwana wa Sadoki akamwambia tena Yoabu: "Liwalo na liwe, tafadhali niruhusu nikimbie na kumfuata yule Mkushi." Hata hivyo, Yoabu akamwambia: "Mwanangu, kwa nini ukimbie wakati huna habari yoyote ya kupeleka?" **23** Lakini bado akasema: "Liwalo na liwe, acha nikimbie." Yoabu akamwambia:

18:18 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

"Kimbia!" Basi Ahimaazi akakimbia kupitia njia ya wilaya ya Yordani,* na hatimaye akampita huyo Mkushi.

24 Daudi alikuwa ameketi kati ya malango mawili ya jiji,^a na mlinzi^b akapanda ukutani hadi juu ya paa la lango. Akatazama na kumwona mtu fulani akikimbia peke yake.

25 Kwa hiyo mlinzi huyo akaita kwa sauti na kumjulisha mfalme. Mfalme akasema: "Ikiwa yuko peke yake, analeta habari." Mtu huyo alipozidi kukaribia, **26** mlinzi akamwona mtu mwingine akikimbia.

Kwa hiyo mlinzi huyo akamwambia mlinda lango: "Tazama! Mtu mwingine anakimbia peke yake!" Mfalme akasema: "Huyo pia analeta habari."

27 Mlinzi akasema: "Naona mtu wa kwanza akikimbia kama Ahimaazi^c mwana wa Sadoki," basi mfalme akasema: "Huyo ni mtu mwema, naye analeta habari njema."

28 Kisha Ahimaazi akamwambia hivi mfalme kwa sauti: "Mambo yote ni sawa!" Ndiipo akamwinamia mfalme kifudufudi. Halafu akasema: "Abarikiwe Yehova Mungu wako, ambaye amewatia mikononi mwako wanaume waliokuasi* bwana wangu mfalme!"^d

29 Hata hivyo, mfalme akauliza: "Je, kijana Absalomu hajambo?" Ahimaazi akajibu: "Niliona vurugu kubwa Yoabu alipomtuma mtumishi wa mfalme na mimi mtumishi wako, lakini sikuelewa maana yake."^e **30** Kwa hiyo mfalme akasema: "Sogea kando, simama hapa." Basi akasogea kando na kusimama hapo.

18:23 *Tnn., "ile wilaya." 18:28 *Tnn., "walioinua mkono wao dhidi yako."

SURA YA 18

a 2Sa 18:4

b 2Fa 9:17

c 2Sa 18:19

d 2Sa 22:47
Zb 144:1

e 2Sa 18:22

Safu ya 2

a 2Sa 18:21

b 2Sa 22:49
Zb 55:18
Zb 94:1
Zb 124:2, 3

c Zb 27:2

d 2Sa 12:10
2Sa 17:14
2Sa 19:1
Met 19:13

SURA YA 19

e 2Sa 18:5
2Sa 18:14

f 2Sa 17:24

g 2Sa 18:33

h 2Sa 3:2-5
2Sa 5:14-16

31 Ndipo yule Mkushi akafika^a na kusema: "Bwana wangu mfalme na apokee habari hizi: Leo Yehova ametekeleza haki kwa kukuweka huru kutoka mikononi mwa wote waliokuasi."^b **32** Lakini mfalme akamuuliza huyo Mkushi: "Je, kijana Absalomu hajambo?" Ndipo Mkushi akajibu: "Maudui wote wa bwana wangu mfalme na wote waliokuasi ili kukudhuru na wawe kama huyo kijana!"^c

33 Jambo hilo likamtaabisha mfalme, akapanda kwenye chumba kilicho paani juu ya lango na kulia, alikuwa akisema hivi huku akitembea: "Mwanangu Absalomu, mwanangu, mwanangu Absalomu! Laiti ningekufa badala yako, Absalomu mwanangu, mwanangu!"^d

19 Yoabu akaletewa habari hii: "Mfalme analia na kumwombolezea Absalomu."^e **2** Basi siku hiyo ushindi* uligeuka na kuwa maombolezo kwa watu wote, kwa sababu walisikia kwamba mfalme alikuwa akimwombolezea mwana wake.

3 Siku hiyo watu wakarudi jijini kimyakimya^f wakiona aibu kama watu waliokimbia kutoka vitani. **4** Mfalme aliufunika uso wake na kuendelea kulia kwa sauti kubwa: "Mwanangu Absalomu! Absalomu mwanangu, mwanangu!"^g

5 Kisha Yoabu akaingia nyumbani kwa mfalme na kumwambia: "Leo umewaibisha watumishi wako wote ambao siku ya leo waliokoa uhai wako,* uhai wa^h wana wako,^h

19:2 *Au "wokovu." 19:5 *Au "nafsi yako." ^hAu "nafsi ya."

mabinti wako,^a wake zako, na masuria wako.^b **6** Unawapenda wale wanaokuchukia na kuwachukia wale wanaokupenda, kwa maana leo umeonyesha wazi kwamba wakuu wako na watumishi wako hawana maana kwako, kwa sababu nina hakika kwamba ikiwa Absalom angekuwa hai leo na sisi sote tuwe tumekufa, ingekuwa sawa kwako. **7** Sasa inuka, toka nje ukawatie moyo* watumishi wako, kwa sababu naapa kwa jina la Yehova kwamba usipotoka nje, hakuna mtu atakayebaki pamoja nawe usiku wa leo. Hili litakuwa jambo baya zaidi kwako kuliko madhara yote yaliyokupata tangu ulipokuwa kijana mpaka sasa.” **8** Basi mfalme akainuka na kwenda kuketi kwenye lango la jiji, na watu wote wakaambiwa hivi: “Sasa mfalme ameketi langoni.” Kisha watu wote wakaja mbele ya mfalme.

Lakini Waisraeli walikuwa wamekimbia, kila mmoja kwenda nyumbani kwake.^c **9** Watu wote katika makabila yote ya Israeli walikuwa wakibishana, wakisema: “Mfalme alituokea kutoka mikononi mwa maadui wetu,^d naye alituokea kutoka mikononi mwa Wafilisti; lakini sasa ameikimbia nchi kwa sababu ya Absalom.”^e **10** Na Absalom, tuliyentia mafuta ili atutawale,^f amekufa vitani.^g Basi sasa, kwa nini hamfanyi lolote kumrudisha mfalme?”

11 Mfalme Daudi akatuma ujumbe huu kwa Sadoki^h na Abiathariⁱ waliokuwa makuhani: “Waambieni wazee wa

19:7 *Tnn., “ukazungumze na moyo wa.”

SURA YA 19

a 2Sa 13:1

b 2Sa 5:13
2Sa 15:16

c 2Sa 18:17

d 1Sa 17:50
1Sa 18:7
1Sa 19:5
2Sa 5:25
2Sa 8:5

e 2Sa 15:14

f 2Sa 15:10,12

g 2Sa 18:14

h 2Sa 8:17
2Sa 15:25
1Fa 1:8i 1Sa 22:20
1Sa 30:7
2Sa 15:24
1Nya 15:11,12

Safu ya 2

a 2Sa 2:4

b 2Sa 17:25
1Nya 2:16,17c 2Sa 8:16
2Sa 18:5,14d Yos 5:9
1Sa 11:14e 2Sa 16:5
1Fa 2:8,9f 2Sa 9:2,10
2Sa 16:1

Yuda,^a ‘Kwa nini muwe wa mwisho kunirudisha mimi mfalme nyumbani kwangu, wakati ujumbe wa Waisraeli wote umenifikia nyumbani kwangu? **12** Ninyi ni ndugu zangu; ninyi ni mfupa wangu na nyama yangu.* Kwa nini muwe wa mwisho kunirudisha mimi mfalme?’ **13** Nanyi mnapaswa kumwambia Amasa,^b ‘Je, wewe si mfupa wangu na nyama yangu? Basi Mungu na aniadhibu, tena vikali, ikiwa hutakuwa mkuu wa jeshi langu kuanzia sasa na kundenlea badala ya Yoabu.’”^c

14 Kwa hiyo aliitaka* miyo ya watu wote wa Yuda wakawa kama mtu mmoja, wakamtumia mfalme ujumbe huu: “Rudi, wewe na watumishi wako wote.”

15 Mfalme akaanza safari ya kurudi, akafika Yordani, na watu wa Yuda wakaja Gilgali^d ili kumpokea mfalme na kumsindikiza kuvuka Yordani. **16** Ndipo Shimei^e mwana wa Gera, Mbenjamini kutoka Bahurimu, akashuka haraka pamoja na watu wa Yuda ili kumpokea Mfalme Daudi, **17** naye alikuwa na wanaueme 1,000 kutoka Benjamini. Pia Siba,^f mtumishi wa nyumba ya Sauli, pamoja na wanawe 15 na watumishi wake 20 wakashuka haraka kwenye Mto Yordani kabla mfalme hajafika. **18** Naye akavuka* kivuko ili kuivusha nyumba ya mfalme na kufanya lolote alilotaka. Lakini Shimei mwana wa Gera akaanguka mbele ya mfalme kifudifudi mfalme

19:12 *Tnn., “nina uhusiano wa damu nanyi.” 19:14 *Tnn., “aliikunja.” 19:18 *Au labda, “Nao wakavuka.”

alipokuwa karibu kuvuka Mto Yordani. **19** Akamwambia mfalme: “Bwana wangu usinione kuwa na hatia, nawe usikumbuke kosa ambalo mimi mtumishi wako nilifanya^a siku ambayo bwana wangu mfalme ulitoka Yerusalemu. Mfalme, usiweke jambo hilo moyoni mwako, **20** kwa sababu mimi mtumishi wako najua vizuri kwamba nime-tenda dhambi; kwa hiyo leo mimi ndiye wa kwanza kutoka katika nyumba yote ya Yosefu kushuka hapa kuja kukupokea bwana wangu mfalme.”

21 Papo hapo Abishai^b mwana wa Seruya^c akasema: “Je, Shimei hapaswi kuuawa kwa sababu hii, kwa kuwa alimtukana mtiwa-mafuta wa Yehova?”^d **22** Lakini Daudi akasema: “Jambo hili linawahusuje, ninyi wana wa Seruya,^e kwamba mtende kinyume cha matakwa yangu? Je, mtu yeyote anapaswa kuuawa leo katika Israeli? Je, sijui kwamba leo mimi ndiye mfalme wa Israeli?” **23** Kisha mfalme akamwambia Shimei: “Hutakufa.” Naye mfalme akamwambia.^f

24 Mefiboshethi,^g mjukuu wa Sauli, akashuka pia kuja kumpokea mfalme. Hakuwa ameosha miguu wala kukata kucha zake wala hakuwa amenyoa masharubu yake wala kufua mavazi yake tangu siku ambayo mfalme aliondoka mpaka siku aliyorudi kwa amani. **25** Alipofika* Yerusalemu kumpokea mfalme, mfalme alimuuliza: “Mefiboshethi, kwa nini hukwe-

19:25 *Au labda, “Alipotoka.”

SURA YA 19

a 2Sa 16:5

b 2Sa 23:18

c 2Sa 2:18

d Kut 22:28
2Sa 16:7
1Fa 21:13

e 2Sa 3:39
2Sa 16:10

f 1Fa 2:8, 9

g 2Sa 9:3, 6
2Sa 16:3, 4

Safu ya 2

a 2Sa 9:9

b 2Sa 4:4

c Law 19:16
2Sa 16:3

d 2Sa 9:7-10

e 2Sa 16:4

f 2Sa 17:27-29
1Fa 2:7

g Met 3:27

h Met 11:25

nda pamoja nami?” **26** Akamjibu: “Bwana wangu mfalme, mtumishi wangu^a alinidanganya. Kwa maana mimi mtumishi wako nilikuwa nimesema, ‘Acha niweke matandiko juu ya punda wangu ili nipande juu yake na kwenda pamoja na mfalme,’ kwa maana mimi mtumishi wako ni kilema.^b **27** Lakini alinichongea kwako bwana wangu mfalme.^c Hata hivyo, wewe bwana wangu mfalme ni kama malaika wa Mungu wa kweli, basi fanya jambo lolote unaloona ni jema kwako. **28** Kwa maana wewe bwana wangu mfalme ungeiangamiza nyumba yote ya baba yangu, lakini uliniruhusu mimi mtumishi wako niwe miongoni mwa wale wanaokula mezani pako.^d Basi nina haki gani ya kuendelea kumlilia mfalme?”

29 Hata hivyo, mfalme akamwambia: “Kwa nini unaendelea kusema hivyo? Nimeamua kwamba wewe na Siba mgawane lile shamba.”^e **30** Ndiipo Mefiboshethi akamwambia mfalme: “Acha achukue shamba lote, kwa sababu sasa bwana wangu mfalme umerudi kwa amani nyumbani kwako.”

31 Kisha Barzilai^f Mgileadi akashuka kutoka Rogelimu mpaka Yordani ili amsindikize mfalme hadi Yordani. **32** Barzilai alikuwa mzee sana, mwenye umri wa miaka 80, naye alimpa mfalme chakula alipokuwa akikaa Mahanaimu,^g kwa maana alikuwa tajiri sana. **33** Basi mfalme akamwambia Barzilai: “Vuka pamoja nami, nami nitakundalia chakula huko Yerusalemu.”^h **34** Lakini Barzilai

akamwambia mfalme: "Ni siku ngapi* zilizobaki za maisha yangu hivi kwamba niende nawe mfalme mpaka Yerusalemu? **35** Leo nina umri wa miaka 80.^a Je, ninaweza kutofautisha kati ya jema na baya? Je, mimi mtumishi wako ninaweza kuonja ladha ya kile ninachokula na kile ninachokunywa? Je, bado ninaweza kusikia sauti za waimbaji wa kiume na wa kike?^b Basi kwa nini mimi mtumishi wako nikuongezee mzigo bwana wangu mfalme? **36** Mimi mtumishi wako nimeridhika kukuleta wewe mfalme mpaka Yordani. Kwa nini, mfalme, unilipe thawabu hii? **37** Tafadhali, niruhusu mimi mtumishi wako nirudi, na acha nife katika jiji letu karibu na kaburi la baba yangu na mama yangu.^c Lakini mtumishi wako Kimhamu ndiye huyu.^d Acha avuke pamoja nawe bwana wangu mfalme, nawe umtendee unaloona ni jema."

38 Basi mfalme akasema: "Kimhamu atavuka pamoja nami, nami nitamtendea ninaloona ni jema; nitakutendea wewe jambo lolote utakaloniomba." **39** Sasa watu wote wakaanza kuvuka Yordani, na mfalme alipovuka alimbusu Barzilai^e na kumbariki; kisha Barzilai akarudi nyumbani. **40** Mfalme alipovuka kwenda Gilgali,^f Kimhamu alivuka pamoja naye. Watu wote wa Yuda na nusu ya watu wa Israeli wakamvusha mfalme.^g

41 Kisha wanaume wote wa Israeli wakaja kwa mfalme na kumuuliza: "Kwa nini ndugu zetu watu wa Yuda walikui-

SURA YA 19

a Zb 90:10

b Mhu 2:8

c Mwa 50:13

d 1Fa 2:7

e Mwa 31:55
1Sa 20:41
Mdo 20:37

f 1Sa 11:14

g 2Sa 2:4

Safu ya 2

a Amu 8:1
Amu 12:1
2Sa 19:15

b Zb 78:68, 70

SURA YA 20

c 2Sa 20:21

d Amu 3:26, 27
2Sa 15:10

e 2Sa 19:43

f 1Fa 12:16

g Met 24:21

h 2Sa 19:15
2Sa 19:41, 42

i 2Sa 5:11

j 2Sa 15:16

ba na kukuleta wewe mfalme na nyumba yako ng'ambo ya Yordani, pamoja na wanau-me wako wote?"^a **42** Wanau-me wote wa Yuda wakawajibu hivi wanaume wa Israeli: "Kwa sababu mfalme ni mtu wa jamaa yetu.^b Kwa nini jambo hili linawakasirisha? Je, tumekula chochote ambacho kime-mgharimu mfalme, au je, tumepewa zawadi?"

43 Hata hivyo, wanaume wa Israeli wakawajibu hivi wanau-me wa Yuda: "Tuna makabila kumi na kwa hiyo tuna haki zaidi kumhusu Mfalme Daudi kuliko ninyi. Kwa nini, basi, mmetutendea kwa dharau? Je, hatukupaswa kuwa wa kwanza kumrudisha mfalme wetu?" Lakini maneno ya wanaume wa Yuda yalikuwa makali zaidi kuliko maneno ya wanaume wa Israeli.

20 Sasa palikuwa na mfan-nya fujo fulani aliyeyitwa Sheba,^c mwana wa Bikri, Mbenjamini. Alipiga pembe^d na kusema: "Hatuna ushirika wote na Daudi, na hatuna urithi wowote katika mwana wa Yese.^e Enyi Waisraeli, kila mtu aende kwa miungu* yake!"^f

2 Basi wanaume wote wa Israeli wakaacha kumfuata Daudi na kuanza kumfuata Sheba mwana wa Bikri;^g lakini wanaume wa Yuda wakashikamana na mfalme wao, kuanzia Yordani mpaka Yerusalemu.^h

3 Mfalme Daudi alipofika nyumbani kwake* huko Yerusalemu,ⁱ aliwachukua wale masuria kumi aliokuwa amewaacha waitunze nyumba yake,^j akawaweka ndani ya

20:1 *Au labda, "katika mahema."

20:3 *Au "katika jumba lake la mfalme."

nyumba chini ya ulinzi. Aliwapa chakula, lakini hakulala nao.^a Walibaki kifungoni mpaka siku walipokufa, nao waliishi kama wajane, ingawa mume wao alikuwa hai.

4 Sasa mfalme akamwambia Amasa:^b "Waite wanaume wa Yuda waje kwangu katika muda wa siku tatu, nawe pia unapaswa kuwepo."

5 Kwa hiyo Amasa akaenda kuwaita wanaume wa Yuda, lakini alichelewa kurudi wakati alioambiwa arudi.

6 Ndipo Daudi akamwambia Abishai:^c "Huenda Sheba^d mwana wa Bikri atatuletea madhara makubwa zaidi kuliko Absalomu.^e Wachukue watumishi wangu mimi bwana wako umfuatie, ili asipate majiji yenye ngome na kutuonyoka."

7 Basi wanaume wa Yoabu,^f Wakerethi, Wapelethi,^g na wanaume wote mashujaa wakaenda kumfuatia; wakaondoka Yerusalemu ili kumfuatia Sheba mwana wa Bikri. **8** Walipokaribia jiwe kubwa lililoko Gibeoni,^h Amasaⁱ akaja kuwapokea. Sasa Yoabu alikuwa amevaa mavazi yake ya vita, naye alikuwa ametia upanga katika ala yake na kufungia kiunoni. Aliposogea mbele, upanga huo ukaanguka.

9 Yoabu akamuuliza Amasa: "Je, hali yako ni njema ndugu yangu?" Kisha Yoabu akamshika Amasa ndevu kwa mkono wa kulia kana kwamba anataka kumbusu. **10** Amasa hakuchukua tahadhari kuhusiana na upanga uliokuwa mkononi mwa Yoabu, basi Yoabu akamchoma tumboni kwa upanga huo,^j na matumbo yake yakamwagika ardhini. Hakuhitaji kumchoma tena; alikufa ali-

SURA YA 20

a 2Sa 16:21, 22

b 2Sa 17:25
2Sa 19:13
1Nya 2:17c 1Sa 26:6
2Sa 10:10
2Sa 23:18
1Nya 18:12

d 2Sa 20:1

e 2Sa 15:12

f 2Sa 8:16

g 2Sa 8:18
2Sa 15:18
1Fa 1:38h Yos 18:21, 25
Yos 21:8, 17i 2Sa 17:25
2Sa 19:13j 2Sa 3:27
1Fa 2:5

Safu ya 2

a 2Sa 20:1

b 1Fa 15:20
2Fa 15:29

pochomwa mara moja. Kisha Yoabu na ndugu yake Abishai wakamfuatia Sheba mwana wa Bikri.

11 Mmoja wa vijana wa Yoabu akasimama karibu na Amasa na kusema: "Yeyote anayemuunga mkono Yoabu na yeyote ambaye ni wa Daudi, na amfuata Yoabu!" **12** Wakati huo wote Amasa alikuwa akigaagaa kwenye damu yake katikati ya barabara. Kijana huyo alipoona kwamba watu wote walikuwa wakisimama hapo, akamwondoa Amasa barabarani na kumpeleka shambani. Kisha akatupa vazi juu yake, kwa sababu aliona kwamba kila mtu aliyefika mahali alipokuwa alisimama. **13** Baada ya kumwondoa barabarani, wanaume wote walimfuata Yoabu ili kumfuatia Sheba^a mwana wa Bikri.

14 Sheba akapita miongoni mwa makabila yote ya Israeli mpaka jiji la Abeli la Bethmaaka.^b Wabikri wakakusanyika pamoja na kumfuata.

15 Yoabu na wanaume wake wakaja na kumzingira katika jiji la Abeli la Bethmaaka na kutengeneza boma kuzunguka jiji hilo, kwani lilikuwa ndani ya boma. Na wanaume wote waliokuwa pamoja na Yoabu walikuwa wakiuharibu ukuta ili kuangusha chini. **16** Na mwanamke fulani mwenye hekima akasema hivi kwa sauti kutoka jijini: "Sikilizeni wanaume, sikilizeni! Tafadhali, mwambieni Yoabu aje hapa, ili niongee naye." **17** Basi Yoabu akamkaribia, kisha mwanamke huo akamuuliza: "Je, wewe ni Yoabu?" Akamjibu: "Ndiyo." Ndipo

mwanamke huyo akamwambia: "Yasikilize maneno yangu mimi kijakazi wako." Yoabu akasema: "Ninasikiliza." **18** Mwanamke huyo akaendelea kusema: "Zamani walikuwa wakisema, 'Acheni watafute ushauri kule Abeli,' na hivyo ndivyo walivyotatua matatizo. **19** Mimi ni mmojawapo wa watu wanaopejanda amani na waaminifu katika Israeli. Unataka kuliharibu jiji ambalo ni kama mama katika Israeli. Kwa nini uangamize* urithi wa Yehova?" **20** Yoabu akamjibu hivi: "Ni jambo nisiloweza kamwe kwazia kwamba niliangamize na kuliharibu. **21** Sivyo ilivyo. Lakini mtu fulani anayeitwa Sheba^b mwana wa Bikiri kutoka eneo lenye milima la Efraim^c amemwasi* Mfalme Daudi. Mkimtoa nje mtu huyo, nitaondoka jijini." Ndi-po mwanamke huyo akamwambia Yoabu: "Haya! Utatupiwa kichwa chake ukutani!"

22 Mara moja mwanamke huyo mwenye hekima akaenda kuzungumza na watu wote, nao wakamkata kichwa Sheba mwana wa Bikri na kukitupa kwa Yoabu. Basi Yoabu akapiga pembe, nao wakatawanyika kutoka kwenye jiji hilo, kila mmoja akarudi nyumbani kwake;^d naye Yoabu akarudi Yerusalemu kwa mfalme.

23 Yoabu alikuwa mkuu wa jeshi lote la Israeli;^e Bena-ya^f mwana wa Yehoyada^g alikuwa mkuu wa Wakerethi na Wapelethi.^h **24** Adoramⁱ alikuwa msimamizi wa wale walioandikishwa kufanya kazi ya kulazimishwa; na Yehoshafa-

20:19 *Tnn., "uumeze." **20:21** *Tnn., "ameinua mkonu wake dhidi ya."

SURA YA 20

a Kut 19:5
Kum 32:9

b 2Sa 20:1

c Yos 17:14, 15
Amu 2:8, 9

d Mhu 9:14, 15
Mhu 9:18

e 2Sa 8:16
2Sa 19:13

f 2Sa 23:20
1Nya 27:5

g 1Nya 12:27

h 2Sa 8:18
2Sa 15:18
1Fa 1:38, 44

i 1Fa 4:6
1Fa 12:18

Safu ya 2

a 1Fa 4:3

b 2Sa 15:27

c 2Sa 17:15
2Sa 19:11
1Fa 4:4

SURA YA 21

d Law 26:18, 20

e Mwa 9:6
Kut 20:13
Hes 35:30, 33

f Yos 9:3, 27

g Mwa 10:15, 16

h Yos 9:15

i Hes 35:31

j 2Sa 21:1

k Hes 25:4
Kum 21:22

l 1Sa 10:26

ti^a mwana wa Ahiludi alifanya kazi ya kuweka kumbukumbu. **25** Sheva alikuwa mwandishi; Sadoki^b na Abiathari^c walikuwa makuhani. **26** Na Ira, Myairi, akawa pia mhudumu mkuu* wa Daudi.

21 Basi katika siku za Daudi kulikuwa na njaa kali^d kwa miaka mitatu mfululizo, kwa hiyo Daudi akamwomba Yehova ushauri, kisha Yehova akasema: "Sauli na nyumba yake wana hatia ya damu, kwa sababu aliwaua Wagibeoni."^e **2** Basi mfalme akawaita Wagibeoni^f na kungea nao. (Sasa, Wagibeoni hawakuwa Waisraeli bali walikuwa Waamori^g waliokuwa wamebaki, na Waisraeli walikuwa wameapa kwamba hawatawaua,^h lakini Sauli akichochea na bidii yake kwa ajili ya watu wa Israeli na Yuda alitaka kuwaangamiza.) **3** Daudi akawauliza Wagibeoni: "Niwafanyie nini, nami nitawalipaje kwa ajili ya mliyotendewa, ili mubariki urithi wa Yehova?" **4** Wagibeoni wakamwambia: "Jambo ambalo Sauli na nyumba yake walitutenda si suala la fedha wala dhahabu;ⁱ wala hatuwezi kumuua mtu yeyote katika Israeli." Daudi akasema: "Nitawafanyia jambo lolote mtakalosema." **5** Wakamwambia mfalme: "Mtu aliyetua na kupanga njama ya kutuangamiza ili tusiishi katika eneo lolote la Israeli^j— **6** tupatie ni wanawe saba. Tutatundi-ka maiti zao*^k mbele za Yehova katika jiji la Gibeai^l la

20:26 *Tnn., "akawa pia kuhani." **21:6** *Tnn., "tutawaanika," yaani, mikono na miguu yao ikiwa imevunjwa.

Sauli, aliyechaguliwa na Yehova.”^a Ndipo mfalme akasema: “Nitawapa.”

7 Hata hivyo, mfalme akamhurumia Mefiboshethi,^b mwana wa Yonathani mwana wa Sauli, kwa sababu ya kiapo ambacho Daudi na Yonathani mwana wa Sauli walikuwa wameapiana mbele za Yehova.^c

8 Basi mfalme akamchukua Armoni na Mefiboshethi, wana wawili ambao Rispa^d binti ya Aya alimzalia Sauli, na wana watano ambao Mikali^e binti ya Sauli alimzalia Adriel^f mwana wa Barzilai, Mmeholathi. **9** Daudi akawapa Wagibeoni wana hao, nao wakatundika maiti zao mlimani mbele za Yehova.^g Wana wote saba walikufa pamoja; waliuwa siku za kwanza za mavuno, mwanzoni mwa mavuno ya shayiri. **10** Kisha Rispa^h binti ya Aya akachukua gunia na kulitandika mwambani tangu mwanzo wa mavuno mpa-ka mvua kutoka mbinguni ili-ponyeshea maiti hizo; haku-ruhusu ndege wa angani wa-tue juu ya maiti hizo wakati wa mchana wala wanyama wa mwituni wazikaribie wakati wa usiku.

11 Daudi akaambiwa mambo ambayo Rispa binti ya Aya suria wa Sauli alikuwa amefanya. **12** Kwa hiyo Daudi akaenda na kuchukua mifupa ya Sauli na mifupa ya Yonathani mwana wake kutoka kwa viongozi* wa Yabesh-gileadi,ⁱ waliokuwa wameiba mifupa hiyo katika uwanja wa jiji la Beth-shani, ambako Wafilisti walikuwa wamewatundika siku ambayo walimuua Sauli juu ya Gilboa.^j

21:8 *Au labda, “Merabu.” 21:12 *Au labda, “wamiliki wa mashamba.”

SURA YA 21

a 1Sa 9:17

b 2Sa 4:4
2Sa 9:10
2Sa 19:24c 1Sa 18:3
1Sa 20:42

d 2Sa 3:7

e 1Sa 18:20
1Sa 25:44
2Sa 3:14
2Sa 6:23

f 1Sa 18:19

g Hes 35:31
Kum 19:21

h 2Sa 3:7

i 2Sa 2:5

j 1Sa 28:4
1Sa 31:1
1Sa 31:11, 12
2Sa 1:6
1Nya 10:8

Safu ya 2

a 2Sa 21:9

b Yos 18:28

c 1Sa 9:1
1Sa 10:11d Yos 7:24-26
2Sa 24:25

e 2Sa 5:17, 22

f Kum 2:11

g 1Sa 17:4, 7
1Nya 11:23

h 2Sa 23:18, 19

i 2Sa 22:19

j 2Sa 18:3

k 1Fa 11:36
1Fa 15:4
2Fa 8:19

l 1Nya 20:4

m 1Nya 11:26, 29
1Nya 27:1, 11

n Mwa 14:5

o 1Nya 20:5

p 1Sa 17:4, 7

13 Akachukua mifupa ya Sauli na mifupa ya Yonathani mwana wake kutoka mlimani, pia wakaikusanya mifupa ya wanaume waliokuwa wameuwa.*^a **14** Kisha wakaizika mifupa ya Sauli na Yonathani mwana wake katika nchi ya Benjamini kule Sela^b katika kaburi la Kishi^c baba yake. Baada ya kufanya kila jambo ambalo mfalme alikuwa ameamuru, Mungu akasikiliza maombi yao ya kumsihi kuhusu nchi.^d

15 Vita vikatokea tena kati ya Wafilisti na Waisraeli.^e Kwa hiyo, Daudi na watumishi wake wakashuka kwenda kupigana na Wafilisti, lakini Daudi akachoka. **16** Mzao wa Warefaimu^f aliyetwa Ishbi-benobu, aliyekuwa na mkuki wa shaba wenye uzito wa shekeli 300*^g na aliyejihami kwa upanga mpya, alikusudia kumuua Daudi. **17** Mara moja Abishai^h mwana wa Seruya akaja kumsaidia,ⁱ akampiga Mfilisti huyo na kumuua. Wakati huo wanaume wa Daudi wakamwapa hivi: “Usiende tena vitani pamoja nasi! Usiizime taa ya Israeli!”^k

18 Baada ya hayo, wakapigana tena na Wafilisti^l kule Gobu. Wakati huo Sibekai^m Mhusa alimuua Safu, aliyekuwa mzao wa Warefaimu.ⁿ

19 Wakapigana tena na Wafilisti^o huko Gobu, na Elhanani mwana wa Yaare-oregimu Mbethlehemu akamuua Goliathi Mgathi, aliyekuwa na mkuki wenye mpini kama mti wa wafumaji wa nguo.^p

21:13 *Tnn., “wameanikwa.” 21:16 *Karibu kilogramu 3.42. Angalia Nyo-geza B14.

20 Vita vikatokea tena huko Gathi, ambako kulikuwa na mwanamume mkubwa isivyo kawaida, mwenye vidole 6 katika kila mkono na vidole 6 katika kila mguu, jumla ya vidole 24; naye pia alikuwa mzao wa Warefaimu.^a **21** Aliendelea kuwadhihaki Waisraeli.^b Basi Yonathani mwana wa Shimei,^c ndugu ya Daudi, akamuua.

22 Watu hao wanne walikuwa wazao wa Warefaimu huko Gathi, na Daudi na watumishi wake ndio waliowaua.^d

22 Daudi akamwambia Yehova maneno ya wimbo huu^e siku ambayo Yehova alimwokoza kutoka mikononi mwa maadui wake wote^f na kutoka mikononi mwa Sauli.^g **2** Akasema:

“Yehova ni jabali langu na ngome yangu^h na Mwo-kozi wangu.ⁱ

3 Mungu wangu ni mwamba wangu,^j ninayemkimbilia,

Ngao yangu^k na pembe* yangu ya wokovu,[#] kimbilio langu salama.^Δ^l

Na mahali pangu pa kukimbilia,^m mwokozi wangu,ⁿ wewe unayeniokoza kutoka katika ukatili.

4 Ninamlilia Yehova, anayestahili kusifiwa, Nami nitaokolewa kutoka kwa maadui wangu.

5 Mawimbi ya kifo yalinizunguka pande zote;^o Mafuriko ya ghafla ya wanaume wasiofaa kitu ya liniogopesha.^p

22:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au “mwokozi wangu mwenye nguvu.” ΔAu “kilele changu salama.”

SURA YA 21

a 1Nya 20:6-8

b 1Sa 17:10, 45
2Fa 19:22c 1Sa 16:9
1Sa 17:13
1Nya 2:13

d Zb 60:12

SURA YA 22

e Kut 15:1
Amu 5:1

f Zb 34:19

g 1Sa 23:14
Zb 18:Uta

h Zb 31:3

i Zb 18:2, 3

j Kum 32:4
1Sa 2:1, 2k Mwa 15:1
Kum 33:29
Zb 3:3l Zb 9:9
Met 18:10

m Zb 59:16

n Isa 12:2
Lu 1:46, 47
Tit 3:4

o Zb 69:14

p Zb 18:4

Safu ya 2

a Zb 116:3, 4

b Zb 18:5

c Zb 142:1
Yon 2:2d Kut 3:7
Zb 18:6
Zb 34:15

e Amu 5:4

f Ayu 26:11

g Zb 18:7-12
Zb 77:18

h Isa 30:27

i Zb 144:5
Isa 64:1j Kum 4:11
1Fa 8:12
Zb 18:9
Zb 97:2k 1Sa 4:4
Zb 80:1
Zb 99:1

l Ebr 1:7

m Ayu 36:29

6 Kamba za Kaburi* zilinzunguka;^a

Mitego ya kifo ilinikabili.^b

7 Katika taabu yangu nilimwita Yehova,^c Niliendelea kumlilia Mungu wangu.

Kisha akiwa katika hekalu lake akaisikia sauti yangu,

Na kilio changu cha kuomba msaada kilifika masikioni mwake.^d

8 Dunia ikaanza kutetemeka na kutikisika huku na huku;^e

Misingi ya mbingu ikasukasuka^f

Nayo ikatikisika huku na huku kwa sababu alikuwa amekasirishwa.^g

9 Moshi ulipanda kutoka katika mianzi ya pua yake, Na moto unaoteketeza kabisa ukatoka kinywani mwake;^h

Makaa ya mawe yanayowaka moto mkali yakatoka kwake.

10 Alizifanya alimbingu ziji-
jijunje alipokuwa akishuka,ⁱ

Na giza zito lilikuwa chini ya miguu yake.^j

11 Alipanda juu ya kerubi,^k akaja akiruka.

Alionekana juu ya mabawa ya kiumbe wa roho.[#]^l

12 Kisha akaweka giza kumzunguka kama kibanda,^m

Katika maji yenye giza na mawingu mazito.

13 Kutoka katika mwangaza ulio mbele zake makaa

22:6 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 22:11 *Au “ya upepo.”

- ya mawe yenye moto mkali yaliwaka.
- 14** Kisha Yehova akaanza ku-nguruma kutoka mbinguni;^a
Aliye Juu Zaidi aliifanya sauti yake isikike.^b
- 15** Alipiga mishale yake^c akawatawanya;
Radi, akawavuruga.^d
- 16** Sakafu ya bahari ikaonekana;^e
Misingi ya nchi ikafunuliwa kwa kemeo la Yehova,
Kwa mlipuko wa pumzi kutoka katika mianzi ya pua yake.^f
- 17** Aliunyoosha mkono wake kutoka juu;
Akanishika na kunivuta kutoka katika maji yenye kina.^g
- 18** Aliniokoa kutoka kwa adui yangu mwenye nguvu,^h
Kutoka kwa wale wanao-nichukia, waliokuwa na nguvu nyingi kuliko mimi.
- 19** Walinikabili katika siku ya msiba wangu,ⁱ
Lakini Yehova alikuwa tegemeo langu.
- 20** Alinitoa nje na kunileta mahali penye usalama;^{*j}
Aliniokoa kwa sababu ali-pendezwa nami.^k
- 21** Yehova hunithawabisha kulingana na uadilifu wangu;^l
Hunilipa kulingana na usafi wa^{*} mikono yangu.^m
- 22** Kwa maana nimezishika njia za Yehova,
Nami sijamwacha kwa uovu Mungu wangu.

22:20 *Au "mahali penye nafasi kubwa."

22:21 *Au "ukosefu wa hatia wa."

SURA YA 22

a Kut 19:16

1Sa 2:10

b Zb 18:13-16

Isa 30:30

c Zb 7:13

Zb 77:17

d Zb 144:6

e Kut 14:21

Zb 106:9

Zb 114:3

f Kut 15:8

g Zb 18:16-19

Zb 124:2-4

Zb 144:7

h Zb 3:7

Zb 56:9

i 1Sa 19:11

1Sa 23:26

2Sa 15:10

j Zb 31:8

k Zb 149:4

l 1Sa 26:23

1Fa 8:32

m Zb 18:20-24

Zb 24:3, 4

Safu ya 2

a Kum 6:1

Zb 19:9

b Kum 8:11

c Zb 84:11

d Zb 18:23

Met 14:16

e Ayu 34:11

Isa 3:10

Ebr 11:6

f Zb 18:24

Met 5:21

g Zb 37:28

Zb 97:10

h Zb 18:25-30

i Mt 5:8

1Pe 1:16

j Zb 125:5

k Ayu 34:28

l Da 4:37

1Pe 5:5

m Zb 27:1

n Zb 97:11

o Zb 18:29

Flp 4:13

Ebr 11:33, 34

p Kum 32:4

q Zb 12:6

Met 30:5

r Zb 35:2

Zb 91:4

23 Hukumu zake zote^a ziko mbele yangu;Sitageuka kando kutoka kwenye sheria zake.^b**24** Nitabaki bila lawama^c mbele zake,Nami nitajiepusha na uovu.^d**25** Yehova na anilipe kulingana na uadilifu wangu,^eKulingana na usafi wangu^{*} mbele zake.^f**26** Kwa mtu mshikamanifu unatenda kwa ushikamanifu;^gKwa mtu asiye na lawama, mtu hodari, unatenda bila lawama;^h**27** Kwa walio safi unajidhihirisha mwenyewe kuwa safi,ⁱLakini kwa waliopotoka unajidhihirisha mwenyewe kuwa mwenye busara.^{*j}**28** Kwa maana wewe huwako wali wanyenyekevu,^kLakini macho yako hayapendezwi na wenye kiburi, nawe huwashusha.^l**29** Kwa maana wewe ni taa yangu, Ee Yehova;^mYehova ndiye anayefanya giza langu liangaze.ⁿ**30** Kwa msada wako ninaweza kukabiliana na kundi la wavamizi;Kwa nguvu za Mungu ninaweza kuupanda ukuta.^o**31** Njia ya Mungu wa kweli ni kamilifu;^pNeno la Yehova ni safi.^qYeye ni ngao kwa wote wanaomkimbilia.^r**22:25** *Au "ukosefu wangu wa hatia."**22:27** *Au labda, "unatenda kama mpumavu."

- 32** Kwa maana ni nani aliye Mungu ila Yehova?^a
Na ni nani aliye mwamba isipokuwa Mungu wetu?^b
- 33** Mungu wa kweli ni ngome yangu imara,^c
Naye ataifanya njia yangu iwe kamilifu.^d
- 34** Huifanya miguu yangu iwe kama ya paa;
Hunifanya nisimame mahali palipo juu.^e
- 35** Huizoeza mikono yangu kupigana vita;
Mikono yangu inaweza kuukunja upinde wa shaba.
- 36** Wewe hunipa ngao yako ya wokovu,
Na unyenyekevu wako hunifanya niwe mkuu.^f
- 37** Unapanua njia kwa ajili ya hatua zangu;
Miguu yangu haitateleza.*^g
- 38** Nitawafuatia maadui wangu na kuwaangamiza;
Sitarudi mpaka watakapoangamizwa kabisa.
- 39** Nami nitawaangamiza kabisa na kuwaponda, hivi kwamba hawatainuka;^h
Wataanguka chini ya miguu yangu.
- 40** Utanipa nguvu kwa ajili ya vita;ⁱ
Utawafanya maadui wangu waanguke chini yangu.^j
- 41** Utawafanya maadui wangu wanikimbia;*^k
Nitawakomesha[#] wale wa-naonichukia.^l
- 42** Wanalilia msaada, lakini hakuna mtu wa kuwako; a

22:37 *Au "Vifundo vya miguu yangu havitateleza." 22:41 *Au "Utanionyesha migongo ya maadui wangu." #Au "Nitawanyamazisha."

SURA YA 22

- a Isa 44:6
b Kum 32:31
Zb 18:31-42
c Zb 27:1
Isa 12:2
d Isa 26:7
e Isa 33:15, 16
Hab 3:19
f Zb 18:35
Zb 113:6-8
g Zb 17:5
h Kut 14:13
i 1Sa 23:5
j 1Sa 17:49
Zb 44:3, 5
k Mwa 49:8
l Zb 18:40

Safu ya 2

- a 1Sa 28:6
Met 1:28
Isa 1:15
Mik 3:4
b 1Sa 30:6
2Sa 15:12
c 2Sa 8:3
Zb 2:8
Zb 60:8
d Zb 18:43-45
e Kum 33:29
f Kum 32:4
g Zb 18:46
Zb 89:26
h 1Sa 25:29
2Sa 18:19
i Zb 18:47
Zb 110:1
Zb 144:1, 2
j 2Sa 5:12
2Sa 7:9
k Zb 18:48
l Kum 32:43
Zb 117:1

- m 1Nya 16:9
Zb 145:2
Ro 15:9

- Hata wanamlilia Yehova, lakini yeye hawajibu.^a
- 43** Nitawaponda wawe laini kama mavumbi ya dunia;
Nitawapondaponda na kuwakanyaga-kanyaga kama matope barabarani.
- 44** Utaniokoa kutoka kwa watu wangu ambao hutafuta makosa.^b
Utanalinda niwe kiongozi wa mataifa;^c
Watu ambao siwajui watanitumikia.^d
- 45** Wageni watakuja wakijikunyata mbele zangu;^e
Watanitii kwa sababu ya mambo watakayosikia kunihusu.*
- 46** Wageni watakosa ujasiri;*
Watakuja wakitetemeka kutoka katika ngome zao.
- 47** Yehova yuko hai! Mwamba wangu na asifiwi!^f
Mungu wa mwamba wa wokovu wangu na akwezwe.^g
- 48** Mungu wa kweli hunilipizia kisasi;^h
Huyatiisha mataifa chini yangu;ⁱ
- 49** Yeye huniokoa kutoka kwa maadui wangu.
Unaniinua juu^j ya wale wa-naonishambulia;
Unaniokoa kutoka kwa mtu mkatili.^k
- 50** Ndiyo sababu nitakushukuru wewe, Ee Yehova, miongoni mwa mataifa,^l
Nami nitaliambia sifa* jina lako:^m

22:45 *Tnn., "Mara tu sikio lao linaposikia, watanitii." 22:46 *Au "watafifia." 22:50 *Au "nitalipigia muziki."

51 Yeye hutenda matendo makuu ya wokovu kwa ajili ya mfalme wake;*^a Humtendea mtiwa-mafuta wake kwa upendo mshikamanifu, Kwa Daudi na kwa uzao wake[#] milele.”^b

23 Haya ndiyo maneno ya mwisho ya Daudi:^c

“Neno la Daudi mwana wa Yese,^d

Na neno la mwanamume aliyeinuliwa juu,^e

Mtiwa-mafuta^f wa Mungu wa Yakobo,

Mwimbaji anayependeza* wa nyimbo^g za Israeli.

2 Roho ya Yehova ilisema kupitia mimi;^h

Neno lake lilikuwa kwenye ulimi wangu.ⁱ

3 Mungu wa Israeli alisema; Mwamba wa Israeli/ ali-niambia:

‘Yule anayetawala wana-damu anapokuwa mwadilifu,^k

Anapotawala kwa kumwogopa Mungu,^l

4 Ni kama mwangaza wa asubuhi jua linapoa-ngaza,^m

Asubuhi isiyo na mawingu. Ni kama mwangaza baada ya mvua kunyesha, Ambao unaotesha majani duniani.’ⁿ

5 Je, sivyo ilivyo nyumba yangu mbele za Mungu?

Kwa maana amefanya pamoja nami agano la milele,^o

Lililopangwa kwa utarati-

SURA YA 22

a Zb 2:6
Zb 21:1

b Zb 89:20, 29
Lu 1:32, 33

SURA YA 23

c Mwa 49:1
Kum 33:1

d 1Sa 17:58
Mt 1:6

e 2Sa 7:8

f 1Sa 16:13

g 1Nya 16:9

h Mk 12:36
2Ti 3:16

i Mdo 1:16
2Pe 1:21

j Kum 32:4
Zb 144:1

k Met 29:2
Isa 9:7
Isa 32:1

l Kut 18:21
Isa 11:3

m Mal 4:2
Mt 17:2
Ufu 1:16

n Zb 72:1, 6

o 2Sa 7:16, 19
1Nya 17:11
Zb 89:3
Zb 89:28, 29
Zb 132:11

Safu ya 2

a Isa 9:7
Isa 11:1
Amo 9:11

b Zb 37:10

c 2Sa 10:7
2Sa 20:7
1Nya 11:10

d 1Nya 11:11

e 1Nya 11:12-14

f 1Nya 27:1, 4

g Amu 8:4

h Amu 15:14, 16
1Sa 14:6
1Sa 19:5

bu katika kila jambo na kuhakikishwa.

Kwa sababu linamaanisha wokovu wangu wote na furaha yangu yote,

Je, yeye halifanyi lisitawi kwa sababu hiyo?^a

6 Lakini watu wasiofaa kitu hutupwa^b wote kama vichaka vya miiba,

Kwa maana hawawezi kuchukuliwa kwa mkono.

7 Mtu anapowagusa,

Anapaswa kujihami kika-mili kwa chuma na mpini wa mkuki,

Nao wanapaswa kuteketezwa kabisa kwa moto mahali walipo.”

8 Haya ndiyo majina ya mashujaa hodari wa Daudi:^c Yosheb-bashebethi Mtakemoni, kiongozi wa wale watatu.^d Wakati mmoja, alitumia mkuki wake kuwaua watu 800. 9 Aliyemfuata ni Eleazari^e mwana wa Dodo^f mwana wa Ahohi, naye alikuwa miongoni mwa mashujaa hao watatu hodari waliokuwa na Daudi walipowadhiki Wafilisti. Walikuwa wamekusanyika huko kwa ajili ya vita, na wanaume wa Israeli walipokimbia, 10 alisimama imara na kuendelea kuwaua Wafilisti mpaka mkono wake ulipochoka na kuganda kwa sababu ya kuushika upanga.^g Basi Yehova akawapa ushindi* mkubwa siku hiyo;^h na watu wakamfuata Eleazari ili kuchukua nyara za watu waliouawa.

11 Aliyemfuata ni Shamma mwana wa Agee, Mharari. Wafilisti walikusanyika kule Lehi, mahali ambapo palikuwa na shamba lililojaa dengu;

22:51 *Au “humpa ushindi mkubwa mfalme wake.” #Tnn., “mbegu yake.”
23:1 *Tnn., “Yule anayependeza.”

23:10 *Au “wokovu.”

na watu wakakimbia kwa sababu ya Wafilisti. **12** Lakini alisimama katikati ya shamba hilo na kuwazuia Wafilisti wasiingie humo, naye aliendelea kuwaua Wafilisti, hivi kwamba Yehova akawapa ushindi* mkubwa.^a

13 Viongozi watatu kati ya wale viongozi 30 walishuka wakati wa mavuno kwenenda kwa Daudi katika pango la Adulamu,^b na kikosi* cha Wafilisti kilikuwa kimepiga kambi katika Bonde la[#] Refaimu.^c **14** Wakati huo Daudi alikuwa ndani ya ngome,^d na kituo cha ulinzi cha Wafilisti kilikuwa Bethlehemu. **15** Kisha Daudi akasema alichotamani: "Laiti ningekunywa maji kutoka tangi lililo karibu na lango la Bethlehemu!" **16** Ndipo wale mashujaa watatu hodari wakaingia kwa nguvu katika kambi ya Wafilisti, wakateka maji kutoka katika tangi hilo lililo karibu na lango la Bethlehemu na kumletea Daudi; lakini akakataa kuyanywa, akayamwaga mbele za Yehova.^e **17** Akasema: "Ni jambo nisiloweza kumwe kuwazia, Ee Yehova, kufanya hivyo! Je, ninywe damu^f ya wanaume walioenda kuhatarisha uhai wao?"* Basi akakataa kuyanywa. Hayo ndiyo mambo walivyotenda mashujaa wake watatu hodari.

18 Abishai^g ndugu ya Yoabu mwana wa Seruya^h alikuwa kiongozi wa wengine watatu; alitumia mkuki wake kuwaua watu 300, naye alikuwa maarufu kama wale watatu.ⁱ **19** Ingawa alikuwa mashu-

SURA YA 23

a Zb 3:8
Zb 44:3

b Yos 15:20, 35
1Sa 22:1

c Yos 15:1, 8
2Sa 5:22
1Nya 11:15-19

d 1Sa 22:1, 4
1Nya 12:16

e Law 9:9
Law 17:13

f Mwa 9:4
Law 17:10

g 1Sa 26:6
2Sa 21:17

h 2Sa 2:18
1Nya 2:15, 16

i 1Nya 11:20, 21

Safu ya 2

a 2Sa 8:18
2Sa 20:23
1Fa 1:8
1Fa 2:29
1Nya 27:5, 6

b Yos 15:21

c 1Nya 11:22-25
Met 30:30

d 2Sa 2:18, 23
1Nya 2:15, 16
1Nya 27:1, 7

e 1Nya 11:26-41

f 1Nya 27:1, 10

g 1Nya 27:1, 9

h 1Nya 27:1, 12

i Yos 21:8, 18
Yer 1:1

j 1Nya 27:1, 13

k 1Nya 27:1, 14

huri zaidi kuliko wale wengine watatu na alikuwa kiongozi wao, hakuwa shujaa kama wale watatu wa kwanza.

20 Benaya^a mwana wa Yehoyada alikuwa mwanamume jasiri* aliyefanya mambo mengi ya kishujaa kule Kabzeeli.^b Aliwaua wana wawili wa Arieli wa Moabu, naye aliingia ndani ya shimo la maji siku ya theluji na kumuua simba.^c **21** Alimua pia mwanamume Mmisri aliyekuwa mkubwa isivyo kawaida. Ingawa Mmisri huyo alikuwa na mkuki mkononi, Benaya alikabiliana naye akiwa na fimbo, akamnyang'anya Mmisri huyo mkuki kutoka mkononi mwake na kumuua kwa mkuki wake mwenyewe. **22** Benaya mwana wa Yehoyada alifanya mambo hayo, naye alikuwa maarufu kama wale mashujaa watatu hodari. **23** Ingawa alikuwa mashuhuri hata kuliko wale 30, hakuwa shujaa kama wale watatu. Lakini Daudi alimweka kuwa kiongozi wa walenzi wake binafsi.

24 Asaheli^d ndugu ya Yoabu alikuwa miongoni mwa wale 30: Elhanani mwana wa Dodo wa Bethlehemu,^e **25** Shamma Mharodi, Elika Mharodi, **26** Helezi^f Mpeleti, Ira^g mwana wa Ikeshi Mtekoa, **27** Abiezeri^h Mwanathothi,ⁱ Mebunai Mhusha, **28** Salmoni Mwahohi, Maharai^j Mnetofa, **29** Helebu mwana wa Baana Mnetofa, Itai mwana wa Ribai wa jiji la Gibeala wa Wabenjamini, **30** Benaya^k Mpirathoni, Hida kutoka katika makorongo*

23:12 *Au "wokovu." 23:13 *Au "kijiji cha mahema." #Au "Nchi Tambarare ya Chini ya." 23:17 *Au "nafsi zao."

23:20 *Tnn., "mwana wa mwanamume jasiri." 23:30 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

ya Gaashi,^a **31** Abi-alboni Mwarbathi, Azmavethi Mbarhumu, **32** Eliaba Mshaalboni, wana wa Yasheni, Yonathani, **33** Shamma Mharari, Ahiamu, mwana wa Sharari Mharari, **34** Elifeleti mwana wa Ahasbai mwana wa yule Mmaakathi, Eliamu mwana wa Ahithofeli^b Mgiloni, **35** Hezro Mkarmeli, Paarai Mwarabi, **36** Igali mwana wa Nathani wa Soba, Bani Mgadi, **37** Seleki Mwamoni, Naharai Mbeerothi, aliyembebea silaha Yoabu mwana wa Seruya, **38** Ira Mwithri, Garebu Mwithri,^c **39** na Uria^d Mhiti—wote waliukuwa 37.

24 Hasira ya Yehova ikawaka tena dhidi ya Waisraeli^e mtu fulani alipomchochea Daudi* atende kinyume chao kwa kumwambia: “Nenda, ukawahesabu^f watu wa Israeli na Yuda.”^g **2** Basi mfalme akamwambia Yoabu^h mkuu wa jeshi aliyekuwa pamoja naye: “Tafadhali nenda katika makabila yote ya Israeli, kuanzia Dani mpaka Beersheba,ⁱ uwaandikishe watu, ili nijue idadi yao.” **3** Lakini Yoabu akamwambia mfalme: “Yehova Mungu wako na azidishe idadi ya watu mara 100, na macho yako bwana wangu mfalme na yaone jambo hilo, lakini kwa nini bwana wangu mfalme unataka kufanya jambo la namna hii?”

4 Lakini neno la mfalme likawa na nguvu kuliko neno la Yoabu na wakuu wa jeshi. Basi Yoabu na wakuu wa jeshi wakaondoka mbele ya mfalme na kwenda kuwaandikisha watu wa Israeli.^j **5** Wa-

24:1 *Au “Daudi alipochochewa.”

SURA YA 23

a Amu 2:8, 9

b 2Sa 15:31

2Sa 16:23

2Sa 17:23

1Nya 27:33

c 1Nya 2:53

d 2Sa 11:3

1Fa 15:5

SURA YA 24

e 2Sa 21:1

f 1Nya 27:23, 24

g 1Nya 21:1-3

h 2Sa 8:16

2Sa 20:23

i Amu 20:1

j Hes 1:2

1Nya 21:4

Safu ya 2

a Kum 2:36

Yos 13:8, 9

b Hes 32:34, 35

c Hes 32:40

d Mwa 10:15

Mwa 49:13

Yos 11:8

e Yos 19:24, 29

f Yos 11:19

g Yos 15:1

h Mwa 21:31

Yos 15:21, 28

i Hes 2:32

Hes 26:51

1Nya 21:5, 6

1Nya 27:23

j 1Sa 24:5

Ro 2:15

k 2Sa 12:13

l Zb 130:3

Ho 14:2

1Yo 1:9

m 1Nya 21:8-13

n 1Sa 22:5

1Nya 29:29

o Met 3:12

p Law 26:18, 20

2Sa 21:1

kavuka Yordani na kupiga kambi Aroeri,^a upande wa kulia* wa jiji katikati ya bonde, nao wakaelekea kwa Wagadi na mpaka Yazeri.^b **6** Kisha wakaenda mpaka Gileadi^c na nchi ya Tahtim-hodshi, wakaelekea mpaka Dani-yaani nao wakazunguka mpaka Sidoni.^d **7** Kisha wakaenda kwenye ngome ya Tiro^e na katika majiji yote ya Wahivi^f na ya Wakanaani, mwishowe wakafika Negebu^g ya Yuda kule Beersheba.^h **8** Kwa hiyo wakapita katika nchi yote na kurudi Yerusalemu baada ya miezi tisa na siku 20. **9** Basi Yoabu akampa mfalme idadi ya watu walioandikishwa. Mashujaa wa Israeli waliojhami kwa mapanga walikuwa 800,000, na wanaume wa Yuda walikuwa 500,000.ⁱ

10 Lakini moyo wa Daudi ukajaa* majuto/ baada ya kuwahesabu watu. Basi Daudi akamwambia Yehova: “Nimetenda dhambi^k kubwa kwa kufanya jambo hili. Na sasa, Yehova, tafadhali nisamehe kosa langu mimi mtumishi wako,^l kwa maana nimetenda kwa upumavu sana.”^m **11** Daudi alipoamka asubuhi, neno la Yehova likamjia nabii Gadi,ⁿ mwonaji wa Daudi, likisema: **12** “Nenda ukamwambie Daudi, ‘Yehova anasema hivi: “Ninakupa mambo matatu ya kuchagua. Chagua jambo nitakalokutendea.””^o **13** Basi Gadi akaenda kwa Daudi na kumwambia: “Je, unataka njaa kali ije katika nchi yako kwa miaka saba?^p Au unataka kuwakimbia maadui wako kwa miezi mitatu huku wakiku-

24:5 *Au “kusini.” 24:10 *Au “dhamiri ya Daudi ikajaa.”

fuatia?^a Au unataka nchi yako ikumbwe na ugonjwa hata-ri kwa siku tatu?^b Sasa fikiri-ria kwa makini jibu ninalo-paswa kumpa Yule aliyenitu-ma.” **14** Kwa hiyo Daudi akamwambia Gadi: “Jambo hilo linanihuzunisha sana. Tafadhali, acha tuanguke mkono-ni mwa Yehova,^c kwa maana rehema zake ni nyingi;^d laki-ni usiniache nianguke mkono-ni mwa mwanadamu.”^e

15 Ndipo Yehova akaleta ugonjwa hatari^f Israeli kuanzia asubuhi mpaka wakati uliowekwa, hivi kwamba watu 70,000 wakafa^g kuanzia Dani mpaka Beer-sheba.^h **16** Malaika alipounyoosha mkono wake kuelekea jiji la Yerusalem ili kuliangamiza, Yehova akaghairi* kwa sababu ya msiba huo,ⁱ akamwambia malaika aliyekuwa akiwaangamiza watu: “Imetosh! Sasa shusha mkono wako.” Malai-ka wa Yehova alikuwa karibu na uwanja wa kupuria nafaka wa Arauna^j Myebusi.^k

17 Daudi alipomwona malaika aliyekuwa akiwaangamiza watu, akamwambia Yehova: “Mimi ndiye niliyetenda dhambi, na mimi ndiye niliyekosea; lakini kondoo hawa^l—wamefanya nini? Tafadhali, acha mkono wako uniaadhibu mimi na nyumba ya baba yangu.”^m

18 Basi Gadi akaenda kwa Daudi siku hiyo na kumwambia: “Panda ukamjengee Yehova madhabahu kwenye uwanja wa kupuria nafaka wa Arauna Myebusi.”ⁿ **19** Basi Daudi akapanda kulingana na neno la Gadi, kama Yehova alivyoamuru. **20** Arauna ali-

24:16 *Au “akahuzunika.”

SURA YA 24

a Law 26:14, 17

b Law 26:16

c Ebr 12:6

d Zb 103:8
Zb 119:156

e 2Nya 28:1, 5

f Hes 16:46
1Nya 27:24

g 1Nya 21:14, 15

h 2Sa 24:2

i Zb 78:38
Yer 26:19
Yoe 2:13

j 2Nya 3:1

k Mwa 10:15, 16
Yos 15:8

l Zb 95:7

m 1Nya 21:16, 17

n 1Nya 21:18-23
2Nya 3:1

Safu ya 2

a Hes 16:46, 47
Hes 25:8
2Sa 24:15

b 1Nya 21:24-28

c Kut 20:25
1Nya 22:1

d 2Sa 21:14
2Nya 33:13

potazama chini na kumwona mfalme na watumishi wake wakija kumwelekea, mara moja Arauna akatoka nje na kumwinamia mfalme kifudufudi. **21** Arauna akamuuliza: “Bwana wangu mfalme kwa nini umekuja kwangu mimi mtumishi wako?” Daudi akamjibu: “Kununua uwanja wako wa kupuria ili nimjengee Yehova madhabahu, ili ugonjwa hatari ambao umewakumba watu ukomeshwe.”^a **22** Lakini Arauna akamwambia Daudi: “Bwana wangu mfalme uchukue na kutoa unachoo-na ni chema.* Ndio hawa ng’ombe kwa ajili ya dhabihu ya kuteketezwa na kifaa cha kupuria nafaka na nira za ng’ombe utakazotumia kama kuni. **23** Ee mfalme, mimi Arauna nimekupa vitu hivi vyote.” Kisha Arauna akamwambia mfalme: “Yehova Mungu wako na akupe kibali.”

24 Hata hivyo, mfalme akamwambia Arauna: “Hapana, ni lazima niunue kwa bei fulani. Sitamtolea Yehova Mungu wangu dhabihu za kuteketezwa ambazo hazinigharimu chochote.” Basi Daudi akanunua uwanja huo wa kupuria nafaka na hao ng’ombe kwa shekeli 50 za fedha.*^b **25** Kisha Daudi akamjengea Yehova madhabahu^c mahali hapo na kutoa dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za ushirika. Ndipo Yehova akakubali maombi ya kusihhi yaliyotolewa kwa ajili ya nchi,^d na ugonjwa hatari uliowakumba Waisraeli ukakomeshwa.

24:22 *Tnn., “kilicho chema machoni pako.” 24:24 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

KITABU CHA KWANZA CHA
WAFALME

YALIYOMO

- 1 Daudi na Abishagi (1-4)
Adoniya atafuta kiti cha ufalme (5-10)
Nathani na Bath-sheba wachukua hatua (11-27)
Daudi aagiza Sulemani atiwe mafuta (28-40)
Adoniya akimbilia kwenye madhabahu (41-53)
- 2 Daudi ampa maagizo Sulemani (1-9)
Daudi afa; Sulemani aketi kwenye kiti cha ufalme (10-12)
Njama ya Adoniya yasababisha auawe (13-25)
Abiathari afukuzwa; Yoabu auawa (26-35)
Shimei auawa (36-46)
- 3 Sulemani amwoa binti ya Farao (1-3)
Yehova amtokea Sulemani katika ndoto (4-15)
Sulemani aomba hekima (7-9)
Sulemani aamua kesi ya mama wawili (16-28)
- 4 Wasimamizi katika utawala wa Sulemani (1-19)
Ufanisi katika utawala wa Sulemani (20-28)
Wakaa kwa usalama chini ya mzabibu na mtini (25)
Hekima na methali za Sulemani (29-34)
- 5 Mfalme Hiram ampaa Sulemani vifaa vya ujenzi (1-12)
Wafanyakazi wa Sulemani walioandikishwa (13-18)
- 6 Sulemani ajenga hekalu (1-38)
Chumba cha ndani zaidi (19-22)
Makerubi (23-28)
Michongo, milango, ua wa ndani (29-36)
Hekalu lakamilishwa kwa muda wa miaka saba hivi (37, 38)
- 7 Majengo yaliyozunguka jumba la Mfalme Sulemani (1-12)
Hiram mwenye ustadi amsaidia Sulemani (13-47)
Nguzo mbili za shaba (15-22)
- Bahari ya madini yaliyoyeyushwa (23-26)
Magari kumi na mabeseni ya shaba (27-39)
Vyombo vya dhahabu vyakamilishwa (48-51)
- 8 Sanduku la agano laletwa hekaluni (1-13)
Sulemani awahutubia watu (14-21)
Sala ya Sulemani ya kuweka wakfu hekalu (22-53)
Sulemani awabariki watu (54-61)
Dhabihu na sherehe ya wakfu (62-66)
- 9 Yehova amtokea tena Sulemani (1-9)
Zawadi ya Sulemani kwa Mfalme Hiram (10-14)
Miradi mbalimbali ya Sulemani (15-28)
- 10 Malkia wa Sheba amtembelea Sulemani (1-13)
Utajiri mwingi wa Sulemani (14-29)
- 11 Wake za Sulemani waugeuza moyo wake (1-13)
Wapinzani wa Sulemani (14-25)
Yeroboamu aahidiwa makabila kumi (26-40)
Sulemani afa; Rehoboamu awekwa kuwa mfalme (41-43)
- 12 Rehoboamu awajibu watu kwa ukali (1-15)
Makabila kumi yaasi (16-19)
Yeroboamu awekwa kuwa mfalme wa Israeli (20)
Rehoboamu aambiwa asipigane na Waisraeli (21-24)
Yeroboamu aanzisha ibada ya ndama (25-33)
- 13 Unabii dhidi ya madhabahu ya Betheli (1-10)
Madhabahu yapasuka (5)
Mtu wa Mungu akosa kutii (11-34)
- 14 Unabii wa Ahiya dhidi ya Yeroboamu (1-20)
Rehoboamu atawala Yuda (21-31)
Shishaki ashambulia (25, 26)
- 15 Abiyamu, mfalme wa Yuda (1-8)
Asa, mfalme wa Yuda (9-24)

- Nadabu, mfalme wa Israeli (25-32)
Baasha, mfalme wa Israeli (33, 34)
- 16 Hukumu ya Yehova dhidi ya Baasha (1-7)
Ela, mfalme wa Israeli (8-14)
Zimri, mfalme wa Israeli (15-20)
Omri, mfalme wa Israeli (21-28)
Ahabu, mfalme wa Israeli (29-33)
Hieli ajenga upya Yeriko (34)
- 17 Nabii Eliya atabiri ukame (1)
Eliya alishwa na kunguru (2-7)
Eliya amtembelea mjane kule Sarefathi (8-16)
Mwana wa mjane afa na kufufuliwa (17-24)
- 18 Eliya akutana na Obadia na Ahabu (1-18)
Eliya apambana na manabii wa Baali kule Karmeli (19-40)
"Kuyumbayumba kati ya maoni mawili" (21)
Ukame wa miaka mitatu na nusu waisha (41-46)
- 19 Eliya akimbia ghadhabu ya Yezebeli (1-8)
- Yehova amtokea Eliya kule Horebu (9-14)
Eliya aambiwa amtie mafuta Hazaeli, Yehu, Elisha (15-18)
Elisha awakwa rasmi kuchukua nafasi ya Eliya (19-21)
- 20 Wasiria wapigana vita dhidi ya Ahabu (1-12)
Ahabu awashinda Wasiria (13-34)
Unabii dhidi ya Ahabu (35-43)
- 21 Ahabu atamani shamba la mizabibu la Nabothi (1-4)
Yezebeli apanga njama ya kumuua Nabothi (5-16)
Ujumbe wa Eliya dhidi ya Ahabu (17-26)
Ahabu ajinyenyekeza (27-29)
- 22 Yehoshafati aungana na Ahabu (1-12)
Mikaya atabiri kwamba watashindwa (13-28)
Roho ya udanganyifu itampumbaza Ahabu (21, 22)
Ahabu auawa huko Ramothi-gileadi (29-40)
Yehoshafati atawala Yuda (41-50)
Ahazia mfalme wa Israeli (51-53)

1 Sasa Mfalme Daudi alikuwa amezeeka,^a umri wake ulikuwa umesonga,* na ingawa walimfunika kwa nguo, hakuweza kupata joto. **2** Kwa hiyo watumishi wake wakamwambia: "Bwana wetu mfalme turuhusu tukutafutie msichana bikira atakayekuhudumia na kukutunza. Atalala mikononi mwako ili bwana wetu mfalme upate joto." **3** Wakatafuta msichana mrembo katika eneo lote la Israeli, wakampata Abishagi,^b Mshunamu,^c wakamleta kwa mfalme. **4** Msichana huyo alikuwa mrembo sana, naye alimhudumia mfalme na kumtunza, la-

1:1 *Tnn., "siku zake zilikuwa zimesonga."

SURA YA 1

a 2Sa 5:4
1Nya 29:26, 27

b 1Fa 2:17, 22

c Yos 19:17, 18

Safu ya 2

a 2Sa 3:2, 4
1Nya 3:1, 2

b 2Sa 15:1

c 2Sa 20:25

d 1Fa 2:22

e 2Sa 8:17

kini mfalme hakufanya naye ngono.

5 Wakati huo, Adoniya^a mwana wa Hagithi alikuwa akijikweza, akisema: "Nitakuwa mfalme!" Alijitengeneza gari, naye akawa na wapanda farasi na wanaume 50 walio-kimbia mbele yake.^b **6** Lakini baba yake hakuwahi kamwe kumkemea* kwa kumuuliza: "Kwa nini umefanya hivi?" Alikuwa pia na sura nzuri sana, na mama yake alimzaa baada ya Absalomu. **7** Alishauriana na Yoabu mwana wa Seruya na kuhani Abiathari,^c nao wakajitolea kumsaidia Adoniya na kumuunga mkono.^d **8** Lakini kuhani Sadoki,^e

1:6 *Au "kumuuliza hisia."

Benaya^a mwana wa Yehoyada, nabii Nathani,^b Shimei,^c Rei, na wale mashujaa hodari wa Daudi^d hawakumuunga mko-no Adoniya.

9 Mwishowe Adoniya akawatoa dhabihu^e kondoo, ng'ombe, na wanyama waliononeshwa, kando ya jiwe la Zohelathi, lililo karibu na En-rogeli, akawaalika ndugu zake wote wana wa mfalme, na wanauame wote wa Yuda watumishi wa mfalme. **10** Lakini hakumwalika nabii Nathani, Benaya na wale mashujaa hodari, wala Sulemani ndugu yake. **11** Ndipo Nathani^f akamuuliza Bath-sheba,^g mama ya Sulemani:^h "Je, hujasikia kwamba Adoniyaⁱ mwana wa Hagithi amekuwa mfalme, na bwana wetu Daudi hajui lolote kuhusu jambo hilo? **12** Sasa, njoo tafadhali, nikupe ushauri, ili uokoe uhai wako mwenyewe na uhai wa* mwana wako Sulemani.^j **13** Nenda kwa Mfalme Daudi ukamuulize, 'Je, bwana wangu mfalme, hukuniapia mimi kijakazi wako, ukisema: "Sulemani mwana wako atakuwa mfalme baada yangu, naye ndiye atakayeketi kwenye kiti changu cha ufalme"?^k Basi kwa nini Adoniya amekuwa mfalme?" **14** Utakapokuwa ukiendelea kuzungumza na mfalme, nitaingia na kuthibitisha maneno yako."

15 Kwa hiyo Bath-sheba akaingia kwa mfalme, katika chumba chake cha faragha. Mfalme alikuwa amezeeka sana, na Abishagi,^l Mshunamu, alikuwa aki-mhudumia mfalme. **16** Kisha Bath-sheba akainama na

1:12 *Au "nafsi yako mwenyewe na nafsi ya."

SURA YA 1

a 2Sa 20:23
1Nya 27:5

b 2Sa 7:2
2Sa 12:1

c 1Fa 4:7,18

d 2Sa 23:8
1Nya 11:10

e 2Sa 15:12

f 2Sa 7:4, 5

g 2Sa 11:3, 27

h 2Sa 12:24

i 2Sa 3:2, 4

j Amu 9:4-6
1Fa 1:21
2Fa 11:1

k 1Nya 22:9
1Nya 28:5
1Nya 29:1

l 1Fa 1:1, 3

Safu ya 2

a 1Fa 1:13
1Nya 22:9,10

b 1Fa 1:5,11

c 1Fa 1:7

d 1Fa 1:9,10

e 1Fa 1:14

f 1Fa 1:5

g 2Sa 15:12

kumsujudia mfalme, mfalme akamuuliza: "Una ombi gani?" **17** Akajibu: "Bwana wangu, wewe ndiye uliyeniapia mimi kijakazi wako kwa jina la Yehova Mungu wako uliposema, 'Sulemani mwana wako atakuwa mfalme baada yangu, na ndiye atakayeketi kwenye kiti changu cha ufalme.'^a **18** Lakini tazama! Adoniya amekuwa mfalme, na bwana wangu mfalme hujui lolote kuhusu jambo hilo.^b **19** Aliwatoa dhabihu ng'ombe dume, wanyama waliononeshwa, na kondoo wengi sana na kuwaalika wana wote wa mfalme na kuhani Abiathari na Yoabu mkuu wa jeshi;^c lakini hakumwalika Sulemani mtumishi wako.^d **20** Na sasa, bwana wangu mfalme, macho yote ya Waisraeli yanakutazama uwaambie ni nani atakayeketi kwenye kiti chako cha ufalme baada yako bwana wangu mfalme. **21** Usipofanya hivyo, mara tu utakapokufa na kuzikwa pamoja na mababu zako bwana wangu mfalme, mimi na mwanangu Sulemani tutaonwa kuwa wasaliti."

22 Na alipokuwa akiendelea kuzungumza na mfalme, nabii Nathani akaingia.^e **23** Mara moja mfalme akaambiwa hivi: "Nabii Nathani amefika!" Akaingia mbele ya mfalme na kumsujudia mfalme mpaka ardhini. **24** Kisha Nathani akasema: "Bwana wangu mfalme, je, ulisema hivi: 'Adoniya atakuwa mfalme baada yangu, na ndiye atakayeketi kwenye kiti changu cha ufalme'?^f **25** Kwa maana leo ameshuka kwenda kuwatoa dhabihu^g ng'ombe dume, wa-

nyama waliononeshwa, na kndoo wengi sana, naye amewaalika wana wote wa mfalme na wakuu wa jeshi na kuhani Abiathari.^a Wako huko wakila na kunywa pamoja naye, nao wanaendelea kusema, 'Mfalme Adoniya na aishi muda mrefu!' **26** Lakini hakunialika mimi mtumishi wako, wala kuhani Sadoki, wala Benaya^b mwana wa Yehoyada, wala Sulemani mtumishi wako. **27** Je, bwana wangu mfalme umeidhinisha jambo hili bila kuniambia mimi mtumishi wako ni nani anayepaswa kuketi kwenye kiti chako cha ufalme baada yako?"

28 Ndipo Mfalme Daudi akajibu: "Niitieni Bath-sheba." Basi akaingia na kusimama mbele ya mfalme. **29** Kisha mfalme akaapa hivi: "Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, aliyeniokoa* kutoka katika mateso yangu yote,^c **30** kama nilivyokuapia kwa jina la Yehova Mungu wa Israeli, nikisema, 'Sulemani mwana wako atakuwa mfalme baada yangu, na ndiye atakayeketi kwenye kiti changu cha ufalme baada yangu!' hivyo ndivyo nitakavyofanya siku ya leo." **31** Ndipo Bath-sheba akainama mpaka ardhini na kumsujudia mfalme na kusema: "Bwana wangu Mfalme Daudi na aishi milele!"

32 Mara moja Mfalme Daudi akasema: "Niitieni kuhani Sadoki, nabii Nathani, na Benaya^d mwana wa Yehoyada."^e Basi wakaja mbele ya mfalme. **33** Mfalme akawaambia: "Nendeni na watumishi wangu, mkampandishe Sulema-

SURA YA 1

a 1Fa 1:5, 7

b 1Nya 27:5

c Zb 71:23
Zb 103:4d 2Sa 20:23
2Sa 23:20
1Nya 27:5

e 1Fa 1:8

Safu ya 2

a 1Fa 1:38
Lu 19:33-35

b 2Nya 32:30

c 1Sa 16:13

d 1Sa 10:1, 24
2Sa 15:10
2Fa 11:12

e 1Nya 28:20

f 1Fa 3:12
1Fa 10:23
Zb 72:8

g 1Nya 27:5

h 2Sa 15:18
1Nya 18:17i 1Fa 1:33
Mt 21:7

j 2Nya 32:30

k Kut 30:23-25
1Sa 16:13

l 2Sa 6:17

m 1Nya 29:22

n 1Sa 4:5

ni mwanangu juu ya nyumbu* wangu mwenyewe,^a mteremsheni hadi Gihoni.^b **34** Kuhani Sadoki na nabii Nathani watamtia mafuta^c huko awe mfalme wa Israeli; kisha pigeni pembe na kusema, 'Mfalme Sulemani na aishi muda mrefu!'^d **35** Kisha mfuatani anaporudi, naye atakuja na kuketi kwenye kiti changu cha ufalme; atakuwa mfalme baada yangu, nami nitamweka rasmi kuwa kiongozi wa Israeli na wa Yuda." **36** Mara moja Benaya mwana wa Yehoyada akamwambia mfalme: "Amina! Yehova Mungu wako bwana wangu mfalme na athibitise jambo hilo. **37** Kama Yehova alivyokuwa pamoja nawe bwana wangu mfalme, na awe pia na Sulemani,^e na Afanye kiti chake cha ufalme kiwe kikuu zaidi kuliko kiti chako cha ufalme, bwana wangu Mfalme Daudi."^f

38 Kisha kuhani Sadoki, nabii Nathani, Benaya^g mwana wa Yehoyada, na Wakerethi na Wapelethi^h wakateremka, nao wakampandisa Sulemani juu ya nyumbu wa Mfalme Daudi,ⁱ wakampeleka Gihoni.^j **39** Kisha Kuhani Sadoki akachukua pembe ya mafuta^k kutoka hemani^l na kumtia mafuta Sulemani,^m nao wakanza kupiga pembe, na watu wote wakanza kusema hivi kwa sauti kubwa: "Mfalme Sulemani na aishi muda mrefu!" **40** Kisha watu wote wakapanda wakimfuata, wakipiga filimbi na kushangilia sana, hivi kwamba dunia ikapasuka na kufunguka kwa sababu ya kelele zao.ⁿ

1:29 *Au "aliyeikomboza nafsi yangu."

1:33 *Au "nyumbu jike."

41 Adoniya na watu wote aliowaalika wakasikia kelele hizo walipokuwa wamemaliza kula.^a Mara tu Yoabu aliposikia sauti ya pembe, akauliza: “Kwa nini kuna kelele za vurugu jijini?” **42** Alipokuwa bado anaongea, Yonathani^b mwana wa kuhani Abiathari akaja. Kisha Adoniya akamwambia: “Ingia, kwa maana wewe ni mtu mwema,* bila shaka unaleta habari njema.” **43** Lakini Yonathani akamjibu Adoniya: “Hapana! Bwana wetu Mfalme Daudi amemweka Sulemani kuwa mfalme. **44** Mfalme alimwagiza aende pamoja na kuhani Sadoki, nabii Nathani, Benaya mwana wa Yehoyada, na Wakerethi na Wapelethi, nao wakampandisha juu ya nyumbu wa mfalme.^c **45** Kisha kuhani Sadoki na nabii Nathani wakamtia mafuta kuwa mfalme huko Gihoni. Halafu wakapanda kutoka huko wakishangilia, nalo jiji limejaa kelele. Hizo ndizo kelele mlizosikia. **46** Isitoshе, Sulemani ameketi kwenye kiti cha ufalme. **47** Na tena, watumishi wa mfalme wamekuja kumpongeza bwana wetu Mfalme Daudi, wakisema, ‘Mungu wako na alifanye jina la Sulemani liwe na fahari kuliko jina lako, na Akifanye kiti chake cha ufalme kiwe kikuu kuliko kiti chako cha ufalme!’ Ndiipo mfalme akainama kitandani. **48** Na pia mfalme akasema, ‘Yehova Mungu wa Israeli na asifiwe, ambaye leo amemchagua mtu wa kuketi kwenye kiti changu cha ufalme na ameruhusu macho yangu mwenyewe yaone jambo hilo!’”

1:42 *Au “anayeheshimiwa.”

SURA YA 1

a 1Fa 1:9, 25

b 2Sa 15:36
2Sa 17:17

c 1Fa 1:33, 34

Safu ya 2

a Kut 21:14
Kut 38:1, 2
1Fa 2:26

b 1Fa 2:23

SURA YA 2

c Kum 31:6
Yos 1:6
1Nya 28:20

d 1Fa 3:7

e Kum 17:18-20
Mhu 12:13

49 Basi watu wote walioalikwa na Adoniya wakaogopa sana, na kila mmoja wao akainuka na kwenda zake. **50** Adoniya aliogopa pia kwa sababu ya Sulemani, basi akaondoka, akaenda na kuzishika kwa nguvu pembe za madhabahu.^a **51** Sulemani akaletewa habari hii: “Tazama! Adoniya anamwogopa Mfalme Sulemani; naye ameshika pembe za madhabahu, akisema, ‘Mfalme Sulemani na aniapie kwanza kwamba hataniua mimi mtumishi wake kwa upanga.’” **52** Ndiipo Sulemani akasema: “Akite nda kwa njia inayofaa, haku na unywele wake hata mmoja utakaoanguka ardhini; lakini akipatikana ametenda uovu,^b lazima afe.” **53** Basi Mfalme Sulemani akaagiza aletwe kutoka kwenye madhabahu. Ndiipo akaingia na kumwinamia Mfalme Sulemani, kisha Sulemani akamwambia: “Nenda nyumbani kwako.”

2 Daudi alipokaribia kufa, alimpa Sulemani mwana-we maagizo haya: **2** “Nakaribia kufa.* Kwa hiyo, uwe imara^c na ujithibitisha kuwa mwanamume.^d **3** Ni lazima utimize wajibu wako kwa Yehova Mungu wako kwa kutembea katika njia zake na kushika maagizo yake, amri zake, sheria zake,^e na vikumbusho vyake kama vilivyoandikwa katika Sheria ya Musa;^e ndipo utakapofanikiwa^f katika kila jambo unalofanya na kila mahali unapogeuka kwenda. **4** Na Yehova atatimiza ahadi aliyotoa kunihusu aliposema hivi:

2:2 *Tnn., “Ninafuata njia ya dunia yote.” 2:3 *Tnn., “maamuzi yake.”
*Au “utakapotenda kwa hekima.”

'Ikiwa wana wako watakazia uangalifu njia yao kwa kute-mbea kwa uaminifu mbele zangu kwa moyo wao wote na kwa nafsi* yao yote,^a hutakosa kamwe mwanamume wa uzao wako atakayeketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli.^b

5 "Pia unajua vizuri jambo ambalo Yoabu mwana wa Seruya alinitendea, jambo alilowatendea wakuu wawili wa majeshi ya Israeli, Abneri^c mwana wa Neri na Amasa^d mwana wa Yetheri. Aliwaua, na hivyo akamwaga damu^e ya vita wakati wa amani, akapaka damu ya vita kwenye mshipi uliokuwa kiunoni mwake na kwenye viatu alivyokuwa amevaa miguuni. 6 Ni lazima utende kulingana na hekima yako, nawe usimruhusu ashuke Kaburini* kwa amani akiwa amezeeka.^f

7 "Lakini watendee wana wa Barzilai^g Mgileadi kwa upendo mshikamanifu, nao wanasaswa kuwa miongoni mwa wale wanaokula mezani pako, kwa maana hivyo ndivyo walivyonisaidia^h nilipomkimbia Absalomu ndugu yako.ⁱ

8 "Pia, Shimei mwana wa Gera, Mbenjamini, kutoka Bahurimu yuko pamoja nawe. Yeye ndiye aliyenitukana vikali siku niliyokuwa nikienda Mahanaimu;^k lakini aliposhuka kuja kunipokea kwenye Mto Yordani, nilimwambia hivi kwa jina la Yehova: 'Sitakuua kwa upanga.'^l 9 Sasa usikose kumwadhibu,^m kwa maana wewe ni mtu mwenye hekima nawe unajua unalopaswa ku-

2:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:6, 9 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:6 #Tnn., "usiruhusu mvi zake zishuke kwa amani Kaburini."

SURA YA 2

a Kum 6:5
2Fa 20:3
2Fa 23:3
2Nya 17:3
Mt 22:37

b 2Sa 7:12, 16
1Fa 8:25
1Nya 17:11
Zb 132:11, 12

c 2Sa 3:27, 30

d 2Sa 17:25
2Sa 20:10
1Nya 2:17

e Hes 35:33
2Sa 3:28

f 2Sa 3:29
1Fa 2:31-34

g 2Sa 19:31

h 2Sa 17:27-29

i 2Sa 15:14

j 2Sa 16:5-7

k 2Sa 17:24

l 2Sa 19:23

m Kut 22:28

Safu ya 2

a 1Fa 2:44, 46

b 2Sa 5:7
1Nya 11:7
1Nya 29:26, 27
Mdo 2:29

c 1Nya 12:23

d 2Sa 5:4, 5

e 2Sa 7:8, 12
1Nya 29:23
2Nya 1:1
Zb 89:36, 37
Zb 132:12

f 1Fa 1:5, 25

g 1Nya 22:9

h 1Fa 1:1, 3

mtendea; usimruhusu azeeke na kushuka Kaburini."^{**#a}

10 Kisha Daudi akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.^b 11 Daudi alitawala Israeli kwa miaka 40. Alitawala Hebron^c kwa miaka 7, na Yerusalemu kwa miaka 33.^d

12 Kisha Sulemani akaketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi baba yake, na ufalme wake ukaimarishwa kabisa hatua kwa hatua.^e

13 Baada ya muda Adoniya mwana wa Hagithi akaja kwa Bath-sheba, mama ya Sulemani. Bath-sheba akamuuliza: "Je, umekuja kwa amani?" Akamjibu: "Ni kwa amani."

14 Adoniya akasema: "Ningependa kukwambia jambo fulani." Basi akamwambia: "Sema." 15 Adoniya akasema: "Unajua vizuri kwamba ufalme ulipaswa kuwa wangu, na Waisraeli wote walitarajia niwe mfalme;^f lakini ufalme uliniponyoka ukawa wa ndugu yangu, kwa maana Yehova ndiye aliyempa.^g 16 Lakini sasa nakuomba jambo moja tu. Usikatae ombi langu." Basi Bath-sheba akamwambia: "Sema."

17 Adoniya akasema: "Tafadhali, mwombe Mfalme Sulemani—kwa maana hawezi kukataa ombi lako—anipe Abishagi,^h Mshunamu, awe mke wangu." 18 Ndipo Bath-sheba akasema: "Sawa kabisa! Nitazungumza na mfalme kwa niaba yako."

19 Kwa hiyo Bath-sheba akaenda kuzungumza na Mfalme Sulemani kwa niaba ya Adoniya. Mara moja mfalme

2:9 #Tnn., "ni lazima ushushe mvi zake Kaburini pamoja na damu."

akainuka ili kumpokea, akamwinamia. Kisha akaketi kwenye kiti chake cha ufalme, akaagiza pia mama yake aletewe kiti cha ufalme, ili aketi upande wake wa kulia. **20** Bath-sheba akasema: "Nina ombi moja dogo. Usikatae ombi langu." Basi mfalme akamwambia: "Mama yangu, sema ombi lako; kwa sababu sitalikataa." **21** Akasema: "Mruhusu Abishagi, Mshunamu, awe mke wa Adoniya ndugu yako." **22** Ndipo Mfalme Sulemani akamjibu mama yake: "Kwa nini unaomba Abishagi Mshunamu awe mke wa Adoniya? Huenda ukamwomba pia ufalme,^a kwa sababu yeye ni ndugu yangu mku-bwa,^b naye anaungwa mkono na kuhani Abiathari na Yoabu^c mwana wa Seruya."^d

23 Kwa hiyo Mfalme Sulemani akaapa hivi kwa jina la Yehova: "Mungu na aniadhibu, tena vikali, ikiwa Adoniya hakuomba jambo hilo akijua kwamba anahatarisha uhai wake.* **24** Na sasa, kwa hakika kama Yehova anavyoishi, ambaye ameniimarisha kabisa^e na kuniketisha kwenye kiti cha ufalme cha Daudi baba yangu na kunijengea nyumba* kama alivyohadi,^f Adoniya atauawa^g leo." **25** Mara moja Mfalme Sulemani akamtuma Benaya^h mwana wa Yehoyada, akatoka na kwenda kumpiga Adoniya, akafa.

26 Mfalme akamwambia kuhani Abiathari:ⁱ "Nenda Anathothi^j kwenye mashamba yako! Unastahili kufa, lakini leo sitakuua kwa sababu uli-

2:23 *Au "dhidi ya nafsi yake." 2:24 *Au "ukoo wa kifalme."

SURA YA 2

a 2Sa 16:21

b 1Nya 3:1, 2, 5

c 2Sa 8:16

d 1Fa 1:7

e 1Nya 22:9, 10

f 2Sa 7:11
1Nya 17:10

g 1Fa 1:51, 52

h 2Sa 8:18
1Fa 1:8
1Nya 27:5i 1Sa 22:20
1Fa 1:7j Yos 21:8, 18
Yer 1:1

Safu ya 2

a 1Sa 23:6
2Sa 15:24
1Nya 15:11, 12

b 1Sa 22:22, 23

c 1Sa 2:31
1Sa 3:12

d Yos 18:1

e 1Fa 1:7

f 2Sa 18:14

g 1Nya 21:29

h Mwa 9:6
Kut 21:14
Hes 35:33
Kum 19:13
1Fa 2:5

beba Sanduku la Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova mbele ya baba yangu Daudi^a na kwa sababu ulishiriki katika mateso yote ya baba yangu."^b

27 Basi Sulemani akamwondoa Abiathari asiendelee kutumikia akiwa kuhani wa Yehova, ili kutimiza neno ambalo Yehova alisema dhidi ya nyumba ya Eli^c kule Shilo.^d

28 Habari hizo zilipomfikia Yoabu—kwa maana Yoabu alikuwa amemuunga mkono Adoniya^e lakini hakuwa amemuunga mkono Absalomu^f—Yoabu akakimbilia katika hema la Yehova^g na kushika kwa nguvu pembe za madhabahu.

29 Kisha Mfalme Sulemani akaambiwa hivi: "Yoabu amekimbilia katika hema la Yehova, na yuko humo kando ya madhabahu." Kwa hiyo Sulemani akamtuma Benaya mwana wa Yehoyada, akisema: "Nenda ukamuue!" **30** Basi Benaya akaenda katika hema la Yehova na kumwambia, "Mfalme anasema hivi: 'Toka nje!'" Lakini Yoabu akasema: "Hapana! Nitafia hapa." Benaya akarudi kwa mfalme na kumwambia: "Hivi ndivyo alivyosema Yoabu, na hivi ndivyo alivyonijibu." **31** Kisha mfalme akamwambia: "Fanya kama alivyosema; muue na umzike, uniondolee mimi na nyumba ya baba yangu damu ambayo Yoabu alimwaga kwa njia isiyoyaki.^h **32** Yehova atamlipiza kwa sababu ya damu aliyomwaga,* kwa sababu bila Daudi baba yangu kujua, aliwapiga na kuwaua kwa upanga

2:32 *Tnn., "atarudisha damu yake juu ya kichwa chake mwenyewe."

wanaume wawili walio waadilifu na bora kuliko yeye, yaani, Abneri^a mwana wa Neri mkuu wa jeshi la Israeli,^b na Amasa^c mwana wa Yetheri, mkuu wa jeshi la Yuda.^d

33 Hatia ya damu yao itakuwa juu ya kichwa cha Yoabu na juu ya kichwa cha uzao* wake milele;^e lakini amani kutoka kwa Yehova na iwe milele juu ya Daudi, uzao* wake, nyumba yake, na kiti chake cha ufalme.” **34** Kisha Benaya mwana wa Yehoyada akapanda kwenda huko, akampiga Yoabu na kumuua, akazikwa nyumbani kwake nyikani. **35** Halafu mfalme akamweka Benaya^f mwana wa Yehoyada kuwa mkuu wa jeshi baada yake, na mfalme akamweka Sadoki^g kuwa kuhani bada-la ya Abiathari.

36 Kisha mfalme akamwita Shimei^h na kumwambia: “Jijengee nyumba Yerusalemu, uishi huko; usitoke huko na kwenda mahali pengine popote. **37** Siku utakapotoka na kuvuka Bonde la Kidroni,ⁱ ujue kwa hakika kwamba utakufa. Damu yako itakuwa juu ya kichwa chako mwenyewe.” **38** Shimei akamwambia mfalme: “Jambo ulilosema si baya. Mimi mtumishi wako nitafanya kama ulivyosema bwana wangu mfalme.” Basi Shimei akakaa Yerusalemu kwa siku nyingi.

39 Lakini baada ya miaka mitatu, watumwa wawili wa Shimei wakatoroka na kwenda kwa Akishi^j mwana wa Maa-ka mfalme wa Gathi. Shimei alipoambiwa, “Tazama! Watumwa wako wameenda Gathi,”

2:33 *Au “wazao.”

SURA YA 2

a 2Sa 3:26, 27

b 2Sa 2:8

c 2Sa 20:10

d 2Sa 17:25

e 2Sa 3:29

f 1Nya 11:24
1Nya 27:5

g 1Sa 2:35
1Nya 6:50, 53
1Nya 12:28
1Nya 16:37, 39
1Nya 24:3

h 1Fa 2:8

i 2Sa 15:23
2Fa 23:6
Yoh 18:1

j 1Sa 21:10
1Sa 27:2

Safu ya 2

a 1Fa 2:38

b 2Sa 16:5, 13

c Zb 7:16
Met 5:22

d Zb 21:6
Zb 72:17

e 1Fa 2:8, 9

f 2Nya 1:1
Met 16:12

SURA YA 3

g Kum 7:3, 4
1Fa 7:8
1Fa 9:24
1Fa 11:1
Ne 13:25-27

h 2Sa 5:7
1Nya 11:7

i 1Fa 7:1

j 1Fa 8:17-19

40 mara moja Shimei akawe-ka matandiko juu ya punda wake, akaenda Gathi kwa Akishi kuwatafuta watumwa wake. Shimei aliporudi kutoka Gathi pamoja na watumwa wake, **41** Sulemani akaambiwa: “Shimei aliondoka Yerusalemu na kwenda Gathi, naye amerudi.” **42** Ndipo mfalme akamwita Shimei na kumuuliza: “Je, sikukuapisha kwa jina la Yehova na kukuonya kwa kusema, ‘Siku utakapotoka hapa na kwenda mahali pengine popote, ujue kwa hakika kwamba utakufa’? Na je, wewe hukuniambia, ‘Jambo ulilosema ni sawa; nitatii?’” **43** Kwa nini basi, hukutii kipo cha Yehova na amri niliyokupa?” **44** Kisha mfalme akamwambia Shimei: “Unajua moyoni mwako madhara yote uliyomtendea baba yangu Daudi,^b basi Yehova atakulipiza kwa sababu ya madhara hayo.*^c **45** Lakini mimi Mfalme Sulemani nitabarikiwa,^d na kiti cha ufalme cha Daudi kitaimarishwa kabisa mbele za Yehova milele.” **46** Ndipo mfalme akamwamuru Benaya mwana wa Yehoyada, basi akatoka nje na kumpiga Shimei, akamuua.^e

Hivyo, ufalme ukaimarishwa kabisa mikononi mwa Sulemani.^f

3 Sulemani alifanya mapatano ya ndoa na Farao mfalme wa Misri. Alimwoa* binti ya Farao^g na kumleta katika Jiji la Daudi^h mpaka alipomaliza kujenga nyumba yake mwenyewe,ⁱ na nyumba ya Yehova,^j na ukuta kuzunguka

2:44 *Tnn., “ataleta madhara hayo juu ya kichwa chako mwenyewe.” 3:1 *Au “Alimchukua.”

Yerusalemu.^a **2** Lakini bado watu walikuwa wakitoa dhabihu mahali pa juu,^b kwa maana kufikia wakati huo nyumba haikuwa imejengwa kwa ajili ya jina la Yehova.^c **3** Sulemani akaendelea kumpenda Yehova kwa kutembea katika sheria za Daudi baba yake, ila tu alikuwa akitoa dhabihu na kufanya matoleo yafuke moshi mahali pa juu.^d

4 Mfalme alienda Gibeoni kutoa dhabihu huko, kwa maana ndipo palipokuwa mahali maarufu* zaidi pa juu.^e Sulemani alitoa dhabihu 1,000 za kuteketewa juu ya madhabahu hiyo.^f **5** Huko Gibeoni, Yehova alimtokea Sulemani katika ndoto usiku na kumwambia: "Niombe unachotaka nikupe."^g **6** Basi Sulemani akasema: "Umemtendea mtumishi wako Daudi baba yangu kwa upendo mwingi mshikamanifu alipokuwa akitembea mbele zako kwa uaminifu na kwa uadilifu na kwa unyoofu wa moyo. Umeendelea kumtendea kwa upendo huo mwingi mshikamanifu mpaka leo hii kwa kumpa mwana aketi kwenye kiti chake cha ufalme."^h **7** Na sasa, Yehova Mungu wangu, umeniweka mimi mtumishi wako niwe mfalme baada ya Daudi baba yangu, ingawa mimi ni kijana* tu na sina uzoefu.ⁱ **8** Mimi mtumishi wako ni miongoni mwa watu wako uliowachagua,^j watu wengi sana hivi kwamba hawawezi kuhesabiwa wala idadi yao kujulikana. **9** Basi nipe mimi mtumishi wako moyo mtiifu ili niwahukumu watu wako,^k ni-

3:4 *Tnn., "pakuu." 3:7 *Au "mvulana mdogo." *Tnn., "na sijui kutoka nje na kuingia ndani."

SURA YA 3

a 1Fa 9:15

b 2Nya 33:17

c Kum 12:5, 6
1Fa 5:3
1Nya 28:6d 1Sa 7:9
1Sa 10:8
1Nya 21:26e 1Nya 16:39, 40
1Nya 21:29

f 2Nya 1:3-6

g 2Nya 1:7-10

h 1Fa 2:1, 4

i 1Nya 29:1
Yer 1:6

j Kut 19:5, 6

k Zb 72:1
Zb 119:34

Safu ya 2

a Ebr 5:14

b Met 15:8

c 1Nya 22:12
1Nya 29:19
2Nya 1:11, 12
Met 16:16d Mhu 1:16
1Yo 5:14e 1Fa 4:29
Met 2:3-5
Yak 1:5

f Mt 12:42

g Zb 84:11
Mt 6:33
Efe 3:20h 1Fa 4:21
Mhu 7:11

i 1Fa 10:23

j 1Fa 15:5

k Zb 21:4
Zb 91:14, 16
Met 3:13, 16

l Law 7:11

tofautishe mema na mabaya,^a kwa sababu ni nani anayeweza kuwahukumu watu hawa wako ambao ni wengi sana?"*

10 Ombi hilo la Sulemani lilimpendeza Yehova.^b **11** Basi Mungu akamwambia: "Kwa kuwa umeomba jambo hili, nawe hukujiombea maisha marefu* wala utajiri wala kuomba maadui wako wafe, lakini uliomba uelewaji wa kusikilia za kesi,^c **12** nitafanya ulilomba.^d Nitakupa moyo wenye hekima na uelewaji,^e hivi kwamba kama vile ambavyo hajawahi kamwe kuwapo mtu mwingine kama wewe kabla yako, hatawahi kamwe kuwapo mtu mwingine kama wewe baada yako.^f **13** Isitoshe, nitakupa vitu ambavyo hukuomba,^g utajiri na utukufu,^h hivi kwamba hatakuwapo mfalme mwingine kama wewe katika maisha yako yote.*ⁱ **14** Nawe ukitembea katika njia zangu kwa kushika masharti yangu na amri zangu, kama Daudi baba yako alivyotembea,^j nitakupa pia maisha marefu."**^k

15 Sulemani alipoamka, aligundua kwamba ilikuwa ndoto. Kisha akaenda Yerusalemu, akasimama mbele ya sanduku la agano la Yehova, akatoa dhabihu za kuteketewa na dhabihu za ushirika^l na kuwaandalia karamu watumishi wake wote.

16 Wakati huo makahaba wawili wakaja kwa mfalme na kusimama mbele yake. **17** Mwanamke wa kwanza akasema: "Tafadhali, bwana wangu, mimi na mwanamke

3:9 *Au labda, "wagumu." Tnn., "wazito." 3:11 *Tnn., "siku nyingi." 3:13 *Tnn., "siku zako zote." 3:14 *Tnn., "nitarefusha siku zako."

huyu tunaishi katika nyumba moja, nami nilizaa mtoto alipokuwa nyumbani. **18** Siku ya tatu baada ya mimi kuzaa mtoto, mwanamke huyu pia alizaa mtoto. Tulikuwa pamoja, sisi wawili tu; hapakuwa na mtu mwingine yeyote nyumbani. **19** Usiku, mwana wa mwanamke huyu akafa, kwa sababu alimlalia. **20** Basi akaamka katikati ya usiku, akamchukua mwanangu kutoka kando yangu mimi kijakazi wako nilipokuwa nimelala usingizi, akamlaza mikononi mwake,* kisha akamlaza mwana wake mfu mikononi mwanangu. **21** Nilipoamka asubuhi ili kumnyonyesha mwanangu, nikaona amekufa. Kwa hiyo nikamchunguza kwa makini, nikagundua kwamba hakuwa mwanangu niliyemzaa." **22** Lakini mwanamke huyu mwingine akasema: "Hapana, aliye hai ni mwanangu na aliyekufa ndiye mwanao!" Lakini mwanamke wa kwanza aliendelea kusema: "Hapana, aliyekufa ndiye mwanao, na mwanangu ndiye aliye hai." Hivyo ndivyo walivyobishana mbele ya mfalme.

23 Mwishowe mfalme akasema: "Huyu anasema, 'Huyu aliye hai ni mwanangu, aliyekufa ni mwanao!' na huyu anasema, 'Hapana, aliyekufa ni mwanao, aliye hai ni mwanangu!'" **24** Mfalme akasema: "Nileteeni upanga." Basi wakamletea mfalme upanga. **25** Kisha mfalme akasema: "Mkateni vipande viwili mtoto aliye hai, mpeni mwanamke mmoja nusu moja na nusu nyingine mpeni mwingine." **26** Mara moja mwana-

Safu ya 2

SURA YA 3

a 1Nya 29:23-25
Zb 72:5

b 1Fa 3:9,10

SURA YA 4

c 2Nya 9:30
Mhu 1:12d 1Nya 6:8
1Nya 27:16, 17e 2Sa 8:17
1Nya 27:32f 2Sa 8:16
2Sa 20:24g 1Fa 1:8
1Fa 2:35
1Nya 27:5

h 1Fa 2:26

i 1Fa 1:9,10

j 2Sa 15:37
1Nya 27:33k 2Sa 20:24
1Fa 5:14
1Fa 12:18

l 1Fa 9:15

mke ambaye ni mama ya mtoto aliye hai akamsihi mfalme, kwa maana alishikwa na huruma kwa ajili ya mwanawe. Akasema: "Tafadhali, bwana wangu! Mpe yeye mtoto aliye hai! Usimuee kamwe." Lakini yule mwanamke mwingine alikuwa akisema: "Hatakuwa wako wala hatakuwa wangu. Acha wamkate vipande viwili!" **27** Ndipo mfalme akasema: "Mpeni mwanamke wa kwanza mtoto aliye hai! Msimuee kamwe, kwa maana yeye ndiye mama yake."

28 Kwa hiyo Waisraeli wote wakasikia kuhusu uamuzi uliofanywa na mfalme, nao wakamwogopa mfalme,^a kwa maana waliona kwamba alikuwa na hekima ya Mungu katika kutekeleza haki.^b

4 Mfalme Sulemani alitawala Israeli yote.^c **2** Hawa ndio waliokuwa maofisa wake wakuu:^{*} Azaria mwana wa Sadoki^d alikuwa kuhani; **3** Elihorefu na Ahiya wana wa Shisha walikuwa waandishi;^e Yehoshafati^f mwana wa Ahiludi alifanya kazi ya kuweka kumbukumbu; **4** Benaya^g mwana wa Yehoyada alikuwa mkuu wa jeshi; Sadoki na Abiathari^h walikuwa makuhani; **5** Azaria mwana wa Nathaniⁱ alikuwa mkuu wa wasaidizi; Zabudi mwana wa Nathani alikuwa kuhani na rafiki ya mfalme;^j **6** Ahishari alikuwa msimamizi wa nyumba; na Adoniramuk^k mwana wa Abda aliwasimamia wale walioandikishwa kufanya kazi ya kulazimishwa.^l

7 Sulemani alikuwa na wasaidizi 12 waliowasimamia Waisraeli wote waliomwandalia

4:2 *Au "wakuu wake."

3:20 *Tnn., "kifuani pake."

chakula mfalme na nyumba yake. Kila mmoja wao alikuwa na jukumu la kuanjaa chakula mwezi mmoja kwa mwaka.^a **8** Haya ndiyo majina yao: Mwana wa Huru, katika eneo lenye milima la Efraimu; **9** mwana wa Dekeri, kule Makazi, Shaalbimu,^b Beth-shemeshi, na Elon-beth-hanani; **10** mwana wa Hese-di, kule Arubothi (alisimamia Soko na nchi yote ya Heferi); **11** mwana wa Abinadabu, katika milima yote ya Dori (Tafathi, binti ya Sulemani, akawa mke wake); **12** Baana mwana wa Ahiludi, kule Taanaki, Megido,^c na eneo lote la Beth-sheani,^d ambalo liko kando ya Sarethani chini ya Yezreeli, kuanzia Beth-sheani mpaka Abel-mehola hadi eneo la Yokmeamu;^e **13** mwana wa Geberi, kule Ramothi-gileadi^f (alisimamia vijiji vya mahema vya Yairi^g mwana wa Manase, vilivyoko Gileadi;^h alisimamia pia eneo la Argobu,ⁱ lililoko Bashani; j majiji makubwa 60 yenye kuta na makomeo ya shaba); **14** Ahinadabu mwana wa Ido, kule Mahanaimu;^k **15** Ahimaazi, kule Naftali (alimwoa Basemathi, binti mwingine wa Sulemani); **16** Baana mwana wa Hushai, kule Asheri na Bealothi; **17** Yehoshafati mwana wa Parua, kule Isakari; **18** Shimei mwana wa Ela, kule Benjamini;^m **19** Geberi mwana wa Uri, katika nchi ya Gileadi,ⁿ nchi ya Sihoni^o mfalme wa Waamori, na ya Ogu^p mfalme wa Bashani. Kulikuwa pia na msaidizi mmoja aliyewasimamia wasaidizi hao wengine wote nchini.

SURA YA 4

a 1Nya 27:1

b Yos 19:42, 48

c 2Fa 23:29

d Yos 17:11
1Sa 31:8, 10

e Yos 21:34

f Kum 4:41-43
1Fa 22:3g Hes 32:41
Kum 3:14

h Hes 32:1

i Kum 3:4

j Yos 13:8, 11

k Mwa 32:1, 2
2Sa 2:8, 9

l 1Fa 1:8

m Yos 18:11

n Yos 17:1

o Hes 21:21

p Kum 3:4

Safu ya 2

a Mwa 22:15, 17

b Mhu 2:24

c Mwa 15:18
Kut 23:31
2Sa 8:3
Zb 72:8-10

d Zb 72:10

e Yos 1:4

f Mwa 10:19

g 1Fa 5:4
1Nya 22:9
Zb 72:7h Kum 17:15, 16
1Fa 10:24-26
2Nya 1:14, 17

20 Watu wa Yuda na Israeli walikuwa wengi sana kama chembe za mchanga kando ya bahari;^a walikuwa wakila na kunywa na kushangilia.^b

21 Sulemani alitawala falme zote kuanzia Mto Efrati^c mpaka nchi ya Wafilisti hadi kwenye mpaka wa Misri. Walimletea Sulemani ushuru na kumtumikia siku zote za maisha yake.^d

22 Chakula cha kila siku cha Sulemani kilikuwa kori 30* za unga laini na kori 60 za unga, **23** ng'ombe 10 waliononeshwa, ng'ombe 20 waliopelekwa malishoni, na kondo 100, pamoja na paa kadhaa, swala, kulungu, na ndege waliononeshwa. **24** Kwa maana alitawala kila kitu upande huu wa Mto Efrati,^e kuanzia Tifsa mpaka Gaza,^f pamoja na wafalme wote upande huu wa Mto Efrati; naye alikuwa na amani katika maeneo yake yote.^g **25** Watu wa Yuda na Israeli waliishi kwa usalama, kila mtu chini ya mzabibu wake mwenyewe na chini ya mtini wake mwenyewe, kuanzia Dani mpaka Beer-sheba, siku zote za Sulemani.

26 Na Sulemani alikuwa na mabanda 4,000* ya farasi wa magari yake ya vita, na farasi^h 12,000.^h

27 Wasaidizi hao walimletea chakula Mfalme Sulemani na pia kila mtu aliyekula mezani pa Mfalme Sulemani. Kila

4:22 *Kori moja ilikuwa sawa na lita 220 (kilogramu 170 hivi). Angalia Nyoongeza B14. **4:24** *Yaani, upande wa magharibi wa Mto Efrati. **4:26** *Idadi hii inapatikana katika baadhi ya hati na pia katika simulizi lingine kama hili. Hati nyingine zinasema mabanda hayo yalikuwa 40,000. "Au "wapanda farasi."

mmoja wao alikuwa na jukumu la kuleta chakula mwezi aliopangiwa na kuhakikisha kwamba hakuna chochote kilichokosekana.^a **28** Walipeleka pia shayiri na majani mahali popote yalipohitajiwa kwa ajili ya farasi na kwa ajili ya farasi waliokokota magari, kila mmoja kulingana na kiasi alichogawiwa.

29 Naye Mungu akampa Sulemani hekima na utambuzi mwingi sana na moyo wenye uelewaji mwingi kama mchanga kwenye ufuo wa bahari.^b **30** Hekima ya Sulemani ilizidi hekima ya watu wote wa Mashariki na hekima yote ya Misri.^c **31** Alikuwa na hekima kuliko mwanadamu mwingine yeyote; alikuwa na hekima kuliko Ethani^d Mwezra na Hemani,^e Kalkoli,^f na Darda, wana wa Maholi; umaarufu wake ulienea katika mataifa yote yaliyomzunguka.^g **32** Alitunga* methali 3,000^h na nyimbo zakeⁱ zilikuwa 1,005. **33** Alizungumza kuhusu miti, kuanzia mwerezi wa Lebanoni mpaka mhisopo/unaomea ukutani; alizungumza kuhusu wanyama,^k ndege,^{*l} viumbe wanaotambaa,^{#m} na samaki. **34** Watu kutoka katika mataifa yote walikuja kuisikia hekima ya Sulemani, pamoja na wafalme kutoka kotekote duniani waliokuwa wamesikia kuhusu hekima yake.ⁿ

5 Mfalme Hiram^o aliposikia kwamba Sulemani ametiwa mafuta kuwa mfalme baada ya baba yake, aliwatuma watumishi wake

4:32 *Au "Alinena." 4:33 *Au "viumbe wanaoruka." #Huenda viumbe hao walitia ndani wanyama wanaotambaa na wadudu.

SURA YA 4

a 1Fa 4:7

b 1Fa 10:23
2Nya 1:10
Met 2:6

c Mdo 7:22

d Zb 89:Uta

e Zb 88:Uta

f 1Nya 2:4, 6

g 1Fa 10:1, 7
Lu 11:31h Met 1:1
Mhu 12:9

i Wim 1:1

j Kut 12:22

k Met 30:30

l Met 30:19

m Met 6:6
Met 30:25

n 2Nya 9:1, 23

SURA YA 5

o Eze 27:3

Safu ya 2

a 2Sa 5:11

b 2Nya 2:3

c 2Sa 7:5
1Nya 22:7, 8

d 1Fa 4:24, 25

e Met 16:7

f 2Sa 7:12, 13
1Nya 22:9, 10
2Nya 2:4

g 1Fa 6:9, 20

h 2Nya 2:8

i 2Nya 2:11, 12

kwa Sulemani, kwa maana sikuzote Hiram^o alikuwa rafiiki ya Daudi.^{*a} **2** Naye Sulemani akamtumia Hiram^o ujumbe huu:^b **3** "Unajua vizuri kwamba baba yangu Daudi hakuweza kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wake kwa sababu ya watu waliopigana vita naye pande zote, mpaka Yehova alipoweka maadui wake chini ya nyayo za miguu yake.^c **4** Lakini sasa Yehova Mungu wangu amenipumzisha pande zote.^d Hakuna yeyote anayenipinga na hakuna jambo lolote baya linalotendeka.^e **5** Kwa hiyo ninakusudia kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wangu, kama Yehova alivyomwahidi baba yangu Daudi, akisema: 'Mwana wako ambaye nitamweka kwenye kiti chako cha ufalme baada yako ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili ya jina langu.'^f **6** Sasa waamuru watu wako wanikatie mierezi ya Lebanoni.^g Watumishi wangu watafanya kazi pamoja na watumishi wako, nami nitawali-pa watumishi wako mishahara kulingana na kiwango utakachoweka, kwa maana unajua kwamba hakuna yeyote kati yetu anayejua kukata miti kama Wasidoni."^h

7 Hiram^o aliposikia maneno ya Sulemani, akashangilia sana na kusema: "Yehova na asifiwe leo, kwa maana amempa Daudi mwana mwenye hekima atawale taifa hili kubwa!"^{*i} **8** Basi Hiram^o akampeleka Sulemani ujumbe huu: "Nimepokea ujumbe ulionitumia. Nitatimiza mambo

5:1 *Au "alimpenda Daudi." 5:7 *Au "lenu watu wengi sana."

yote unayotaka ili upate mbao za mierezi na za miberoshi.^a **9** Watumishi wangu watatere-msha magogo kutoka Lebanoni hadi baharini, nami nitaya-funga magogo hayo mafungu-mafungu ili yaelee baharini mpaka mahali utakaponia-ambia. Nitaagiza yafunguliwe, kisha unaweza kuyabeba. Na wewe utanipa chakula nitaka-choomba kwa ajili ya nyumba yangu.”^b

10 Basi Hiram akampa Sulemani mbao zote za mierezi na za miberoshi ambazo Sulemani alihitaji. **11** Naye Sulemani akampa Hiram kori 20,000* za ngano kuwa chakula kwa ajili ya nyumba yake na kori 20 za mafuta bora sana ya zeituni.” Hivyo ndivyo vitu ambavyo Sulemani alimpa Hiram mwaka baada ya mwaka.^c **12** Yehova akampa Sulemani hekima, kama Alivyo-kuwa amemwahidi.^d Na kuli-kuwa na amani kati ya Hiram na Sulemani, nao wakafanya mkataba* kati yao.

13 Mfalme Sulemani ali-waandikisha wanaume kutoka katika Israeli yote ili wafanye kazi ya kulazimishwa; wanaume 30,000 waliandikishwa.^e **14** Alikuwa akiwapeleka wanaume 10,000 Lebanoni kila mwezi kwa zamu. Walikaa Lebanoni kwa mwezi mmoja na kukaa nyumbani kwa miezi miwili; na Adoniram^f ali-wasimamia wale walioandiki-shwa kufanya kazi ya kulazi-mishwa. **15** Sulemani aliku-wa na vibarua* 70,000 na watu

5:11 *Kori moja ilikuwa sawa na kita 220 (kilogramu 170 hivi). Angalia Nyongeza B14. ^aTnn., “za mafuta yali-yopondwapondwa.” 5:12 *Au “agano.” 5:15 *Au “wabeba mizigo.”

SURA YA 5

a 2Sa 6:5
1Fa 6:15
2Nya 3:5

b 2Nya 2:15, 16
Ezr 3:7

c 2Nya 2:10

d 1Fa 3:12
1Fa 4:29
Yak 1:5

e 1Fa 9:15

f 2Sa 20:24
1Fa 4:6
1Fa 12:18

Safu ya 2

a 1Nya 22:15

b Yos 16:10
1Fa 9:20-22
2Nya 2:2
2Nya 2:17, 18
2Nya 8:7-9

c 1Fa 9:23

d 1Fa 7:9
1Nya 22:2

e 1Fa 6:7

f Ufu 21:14

g Yos 13:1, 5

SURA YA 6

h Kut 12:14, 51

i 1Fa 6:37

j 1Nya 28:11, 12
2Nya 3:1, 2

k 2Nya 3:3
Ezr 6:3

l 2Nya 3:4

m Eze 41:26

n Law 16:2
2Nya 5:7
Ebr 9:3

80,000 waliokata mawe^a mili-mani,^b **16** na pia wakuu wa-saidizi^c 3,300 waliowasimamia wafanyakazi. **17** Kwa agizo la mfalme, walichimbua mawe makubwa, mawe yenye thamani,^d ili yachongwe^e na kutumiwa kujenga msingi^f wa nyumba hiyo. **18** Kwa hiyo wajenzi wa Sulemani na wajenzi wa Hiram na Wageba-li^g walikata mawe, na kutay-risha mbao na mawe ya kujen-gea nyumba hiyo.

6 Katika mwaka wa 480 baa-da ya Waisraeli* kutoka katika nchi ya Misri,^h mwaka wa nne baada ya Sulemani ku-wekwa kuwa mfalme wa Israe-li, mwezi wa Zivuⁱ (yaani, mwezi wa pili), Sulemani alia-nza kujenga nyumba ya Yehova.^{aj} **2** Nyumba ambayo Mfalme Sulemani alimjen-gea Yehova ilikuwa na ure-fu wa mikono 60,^{*} upana wa mikono 20, na kimo cha miko-no 30.^k **3** Ukumbi^l wa mbele wa hekalu* ulikuwa na urefu[#] wa mikono 20, nao ulilingana na upana wa nyumba. Uliku-wa na kina cha mikono kumi kuanzia mbele ya nyumba.

4 Aliitengenezea nyumba hiyo madirisha yenye viunzi ambavyo ukubwa wake ulipu-ngua kutoka nje kwenda nda-ni.^m **5** Pia, alijenga jengo la kando lililokaribiana na ukata wa nyumba hiyo; jengo hilo lilizunguka kuta za nyumba hiyo, kuta za hekalu* na za chumba cha ndani zaidi,ⁿ naye

6:1 *Tnn., “wana wa Israeli.” ^aAngalia Nyongeza B15. ^bAngalia Nyongeza B8.

6:2 *Mkono mmoja ulilingana na senti-mita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. 6:3 *Tnn., “hekalu la nyumba.” [#]Au “upana.” 6:5 *Yaani, Patakatifu.

akajenga vyumba vya pembeni kuzunguka pande zote.^a **6** Ghorofa ya chini ya vyumba hivyo vya pembeni ilikuwa na upana wa mikono mitano, ghorofa ya katikati ilikuwa na upana wa mikono sita, na ghorofa ya tatu ilikuwa na upana wa mikono saba, kwa maana aliacha sehemu zilizozingia ndani ukutani kuzunguka nyumba yote, ili kitu chochote kisifungwe kwenye kuta za nyumba hiyo.^b

7 Nyumba hiyo ilijengwa kwa mawe ya machimboni ambayo tayari yalikuwa yamechongwa,^c hivi kwamba hakuna nyundo wala mashoka wala kifaa chochote cha chuma kilichosikika katika nyumba hiyo ilipokuwa ikijengwa. **8** Mlango wa ghorofa ya chini ulikuwa upande wa kusini* wa nyumba hiyo,^d na ngazi iliyopindapinda ilielekea kwenye ghorofa ya katikati, na kutoka ghorofa ya katikati mpaka ghorofa ya tatu. **9** Aliendelea kujenga nyumba hiyo na kuikamilisha,^e akaifunika nyumba hiyo kwa maboriti ya mierezi na safu za mbao za mierezi.^f **10** Alijenga vyumba vya pembeni kuzunguka,^g kila chumba kilikuwa na kimo cha mikono mitano, navyo viliunganishwa kwenye nyumba hiyo kwa mbao za mierezi.

11 Wakati huo, neno hili la Yehova lilimjia Sulemani: **12** "Kuhusu nyumba hii unayojenga, ikiwa utatembea katika maagizo yangu na kutekeleza sheria zangu* na kushika amri zangu zote kwa ku-

6:8 *Tnn., "kulia." 6:12 *Tnn., "maamuzi yangu."

SURA YA 6

a 1Fa 6:10
Eze 41:5,26

b Eze 41:6,7

c 1Fa 5:17

d Eze 41:11

e 1Fa 6:38

f 1Fa 5:6
1Fa 6:20

g 1Fa 6:5

Safu ya 2

a Kum 17:18,19
1Fa 8:25
1Nya 28:9

b 2Sa 7:13
1Nya 22:9

c Kut 25:8
Law 26:12
Zb 132:13

d 1Nya 28:20

e 1Fa 5:8
2Nya 3:5

f 1Fa 6:5

g 2Nya 3:8,9
Ebr 9:3

h Ebr 9:2

i 1Fa 7:24

j Kut 25:33

k Ebr 9:3

l Kut 40:21
1Fa 8:6

m 1Fa 6:16

n Kut 30:1
1Fa 7:48

zifuata,^a mimi pia nitakutimizia ahadi yangu niliyomwahidi baba yako Daudi,^b **13** nami nitakaa miongoni mwa Waisraeli,^c nami sitawaacha watu wangu Waisraeli."^d

14 Sulemani akaendelea kujenga nyumba hiyo ili aikamilishe. **15** Alijenga kuta za ndani za nyumba hiyo kwa mbao za mierezi. Alifunika kuta za ndani kwa mbao, kuanzia sakafu ya nyumba mpaka kwenye maboriti ya dari, akaifunika sakafu yake kwa mbao za miberoshi.^e **16** Na upande wa nyuma wa nyumba hiyo alijenga sehemu fulani yenye ukubwa wa mikono 20 kwa mbao za mierezi, kuanzia sakafuni mpaka kwenye maboriti, na ndani yake* akajenga chumba cha ndani zaidi,^f yaani, Patakatifu Zaidi.^g **17** Na hekalu*^h—sehemu ya nyumba iliyokuwa mbele ya Patakatifu Zaidi—lilikuwa mikono 40. **18** Mbao za mierezi zilizokuwa ndani ya nyumba hiyo zilikuwa na michongo ya vibuyuⁱ na maua ya-ilyochanua.^j Sehemu yote ilifunikwa kwa mbao za mierezi; hakuna jiwe ambalo lilionekana.

19 Naye akatayarisha chumba cha ndani zaidi^k katika nyumba hiyo ili kuweka humo sanduku la agano la Yehova.^l **20** Chumba hicho cha ndani zaidi kilikuwa na urefu wa mikono 20, upana wa mikono 20, na kimo cha mikono 20;^m naye akaifunika kwa dhahabu safi; akaifunika madhabahuⁿ kwa mbao za mierezi.

6:16 *Yaani, ndani ya nyumba hiyo.

6:17 *Yaani, Patakatifu, palipokuwa mbele ya Patakatifu Zaidi.

21 Sulemani aliifunika sehemu ya ndani ya nyumba hiyo kwa dhahabu safi,^a naye akaweka minyororo ya dhahabu kutoka upande mmoja hadi mwingine mbele ya chumba hicho cha ndani zaidi^b kilichokuwa kimefunikwa kwa dhahabu. **22** Aliifunika nyumba yote kwa dhahabu mpaka nyumba yote ilipokamilika; pia aliifunika kwa dhahabu madhabahu yote^c iliyokuwa karibu na chumba cha ndani zaidi.

23 Katika chumba cha ndani zaidi alitengeneza makerubi wawili^d kwa mbao za msonobari,* kila kerubi alikuwa na kimo cha mikono kumi.^e **24** Bawa moja la kerubi lilikuwa na urefu wa mikono mitano, na bawa lingine lilikuwa na urefu wa mikono mitano. Urefu kutoka ncha ya bawa moja mpaka ncha ya bawa lingine ulikuwa mikono kumi. **25** Kerubi wa pili alikuwa pia na kimo cha mikono kumi. Makerubi wote wawili walikuwa na ukubwa uleule na umbo lilelile. **26** Kimo cha kerubi mmoja kilikuwa mikono kumi, sawa na kimo cha kerubi wa pili. **27** Kisha akawaweka makerubi^f hao ndani ya chumba cha ndani zaidi cha nyumba hiyo.* Mabawa ya makerubi hao yalikusuliwa hivi kwamba bawa la kerubi moja lilifika kwenye ukuta mmoja na bawa la kerubi mwingine lilifika kwenye ukuta wa pili, na mabawa yao yalipanuka kuelekea katikati ya nyumba hiyo, hivi kwamba yaligusana. **28** Naye aliwafunika makerubi hao kwa dhahabu.

6:23 *Tnn., "mti wa mafuta," labda ni msonobari wa Aleppo. 6:27 *Yaani, Patakatifu Zaidi.

SURA YA 6

a Kut 26:29
2Nya 3:7

b Kut 26:33

c Kut 30:1,3
Kut 40:5

d Mwa 3:24
2Fa 19:15
Zb 99:1

e 2Nya 3:10-13
2Nya 5:8

f Zb 80:1
Isa 37:16
Ebr 9:4, 5

Safu ya 2

a 2Nya 3:14

b Eze 41:17, 18

c Kut 25:33
1Fa 6:18

d Eze 41:24, 25

e Kut 27:9
2Nya 4:9
2Nya 7:7

f 1Fa 7:12

g 1Fa 6:1

29 Na kwenye kuta zote kuzunguka nyumba hiyo katika vyumba vyote vya ndani na vya nje, alichonga makerubi,^a mitende,^b na maua yaliyochanua.^c **30** Aliifunika sakafu ya nyumba hiyo kwa dhahabu katika vyumba vya ndani na vya nje. **31** Na aliitengeneza milango ya chumba cha ndani zaidi kwa mbao za msonobari, na pia nguzo za pembeni, na miimo yake, ikiwa sehemu ya tano.* **32** Alitengeneza milango hiyo miwili kwa mbao za msonobari, na kwenye milango hiyo alichonga makerubi, mitende, na maua yaliyochanua, kisha akaifunika kwa dhahabu; akawafunika makerubi hao na mitende hiyo kwa dhahabu akitumia nyundo. **33** Hivyo ndivyo alivyotengeneza miimo ya mlango wa hekalu[#] iliyokuwa ya mbao za msonobari, zilikuwa sehemu ya nne.* **34** Naye alitengeneza milango miwili kwa mbao za mberoshi. Mlango mmoja ulikuwa na bawaba mbili ambazo zilizunguka kwenye maegemeo, na mlango mwingine ulikuwa na bawaba mbili ambazo zilizunguka kwenye maegemeo.^d **35** Alichonga makerubi, mitende, na maua yaliyochanua, na kufunika michongo hiyo kwa bamba jembamba la dhahabu.

36 Alijenga ua wa ndani^e kwa safu tatu za mawe yaliyochongwa na safu ya maboriti ya mierezi.^f

37 Katika mwaka wa nne, mwezi wa Zivu,* msingi wa nyumba ya Yehova ulijengwa;^g

6:31, 33 *Huenda inarejelea ujenzi wa kiuuzi cha mlango au ukubwa wa mlango. 6:33 #Yaani, Patakatifu. 6:37 *Angalia Nyongeza B15.

38 na katika mwaka wa 11, mwezi wa Buli,* (yaani, mwezi wa nane), kila kitu katika nyumba hiyo kilikamilishwa kulingana na ramani yake.^a Basi alijenga kwa miaka saba.

7 Sulemani alijenga nyumba yake mwenyewe*^b kwa miaka 13, mpaka alipoikamilisha nyumba yake yote.^c

2 Naye alijenga Nyumba ya Msitu wa Lebanoni^d yenye urefu wa mikono 100,* upana wa mikono 50, na kimo cha mikono 30 juu ya safu nne za nguzo za mierezi; na boriti za mierezi^e zilikuwa juu ya nguzo hizo. **3** Nayo ilifuniwa juu kwa mbao za mierezi zilizokuwa juu ya mihimili iliyolala juu ya nguzo hizo; mihimili hiyo ilikuwa 45, kila safu ilikuwa na mihimili 15. **4** Kulikuwa na safu tatu za madirisha yenye viunzi, na kila dirisha lilielekeana na dirisha lingine katika mistari mitatu. **5** Milango yote na miimo ya milango ilikuwa na viunzi vya mraba,* na sehemu ya mbele ya madirisha yaliyoelekeana katika mistari mitatu ilikuwa pia ya mraba.

6 Naye alijenga Ukumbi wa Nguzo wenye urefu wa mikono 50 na upana wa mikono 30, na mbele yake kulikuwa na ukumbi mwingine wenye nguzo na paa dogo lililochomoza mbele.

7 Alijenga pia Ukumbi wa Kiti cha Ufalme^f ambamo alisikiliza kesi—Ukumbi wa Hukumu^g—nao waliufunika kwa mbao za mierezi kuanzia saka-funi mpaka kwenye maboriti.

6:38 *Angalia Nyongeza B15. 7:1 *Au "jumba lake la mfalme." 7:2 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. 7:5 *Au "mstatili."

SURA YA 6

a 1Nya 28:11, 12

SURA YA 7

b 1Fa 9:10

c Mhu 2:4, 5

d 1Fa 10:16, 17
Isa 22:8

e 1Fa 5:8

f 1Fa 10:18
Zb 122:2, 5g 1Fa 3:9, 28
Met 20:8

Safu ya 2

a 2Fa 20:4

b 1Fa 3:1
1Fa 9:24
2Nya 8:11

c 1Fa 5:17

d 2Nya 4:9

e 1Fa 6:36
2Nya 4:9
2Nya 7:7

f 1Fa 6:3

g 1Fa 7:40
2Nya 2:13, 14

h 2Nya 4:16

i Kut 36:1

8 Nyumba* ambamo angeishi, katika ule ua mwingine,^a ilijengwa nyuma mbali na Ukumbi,^b na muundo wake ulifanana na wa majengo mengine. Alimjengea pia binti ya Farao nyumba iliyofanana na Ukumbi huo; Sulemani alikuwa amemwoa binti huyo.^b

9 Majengo hayo yote yalijengwa kwa mawe ghali^c yaliyochongwa kwa vipimo, yaliyokatwa ndani na nje kwa misumeno ya mawe, kuanzia kwenye msingi mpaka juu ya ukuta, na upande wa nje mpaka kwenye ule ua mkuu.^d

10 Na msingi ulijengwa kwa mawe makubwa sana na yaliyo ghali; baadhi ya mawe yalikuwa na ukubwa wa mikono kumi, na mawe mengine mikono minane. **11** Na juu ya mawe hayo kulikuwa na mawe ghali, yaliyochongwa kwa vipimo, na pia mbao za mierezi. **12** Ua mkuu ulizungukwa na ukuta wenye safu tatu za mawe yaliyochongwa na safu ya maboriti ya mierezi, kama ulivyokuwa ua wa ndani^e wa nyumba ya Yehova na ukumbi wa nyumba.^f

13 Mfalme Sulemani akawatama watu wamwite Hiram,^g akaletwa kutoka Tiro.

14 Alikuwa mwana wa mwana namke mjane kutoka katika kabila la Naftali, na baba yake alikuwa mfua shaba^h kutoka Tiro; Hiram alikuwa na ustadi wa hali ya juu, uelewaji,ⁱ na uzoefu wa kutengeneza vitu vya shaba vya kila aina. Basi akaja kwa Mfalme Sulemani na kufanya kazi yake yote.

7:8 *Au "Jumba la mfalme." ^hTnn., "nyumba ya Ukumbi."

15 Alitengeneza nguzo mbili kwa kutumia shaba iliyoyeyushwa;^a kila nguzo ilikuwa na urefu wa mikono 18, na kila moja ya nguzo hizo mbili ingeweza kuzungukwa kwa kamba yenye urefu wa mikono 12.^{*b}

16 Naye alitumia shaba iliyoyeyushwa kutengeneza vifuniko viwili ambavyo vingeweza juu ya nguzo hizo. Kifuniko kimoja kilikuwa na urefu wa mikono mitano, na kingine kilikuwa na urefu wa mikono mitano. 17 Kifuniko cha kila nguzo kilikuwa na wavu uliofumwa wa minyororo;^c nguzo moja ilikuwa na nyavu saba na nguzo nyingine nyavu saba. 18 Naye alitengeneza safu mbili za makomamanga kuzunguka wavu uliofunika vifuniko vilivyokuwa juu ya nguzo; alifanya hivyo kwa kila nguzo. 19 Vifuniko vilivyokuwa juu ya nguzo za ukumbi vilikuwa na umbo la yungiyungi, na urefu wake ulikuwa mikono minne. 20 Vifuniko hivyo vilikuwa juu ya zile nguzo mbili, juu tu ya sehemu ya mviringo iliyoungana na zile nyavu; na kulikuwa na safu za makomamanga 200 kuzunguka kila kifuniko cha nguzo.^d

21 Alisimamisha nguzo za ukumbi wa hekalu.^{*e} Alisimamisha nguzo ya kulia^f na kuiita Yakini,^Δ kisha akasi-mamisha nguzo ya kushoto[⊠] na kuiita Boazi.^{□f} 22 Sehemu ya juu ya nguzo hizo ilikuwa na umbo la yungiyungi.

7:15 *Au "na kila moja ya nguzo hizo mbili ilikuwa na mzingo wa mikono 12." 7:21 *Yaani, Patakatifu. #Au "ya kusini." ΔMaana yake "Naye [yaani, Yehova] Aimarisha Kabisa." ⊠Au "ya kaskazini." □Labda inamaanisha "Katika Nguvu."

SURA YA 7

a 1Fa 7:21

b 2Fa 25:13, 17
2Nya 3:15
Yer 52:21c 2Fa 25:17
2Nya 4:12, 13d 2Fa 25:17
2Nya 3:16
Yer 52:22, 23e 1Fa 6:3
Eze 40:48

f 2Nya 3:17

Safu ya 2

a Kut 30:18
2Fa 25:13

b 2Nya 4:2-5

c 1Fa 6:18

d Yer 52:20

e 2Fa 25:16
Yer 52:17

Basi kazi ya kutengeneza nguzo ikakamilika.

23 Kisha akatengeneza Bahari* kwa madini yaliyoyeyushwa.^a Ilikuwa ya mviringo, yenye upana wa mikono 10 ukingo hadi ukingo na kimo cha mikono 5, na ingeweza kuzungukwa na kamba yenye urefu wa mikono 30.^{*b}

24 Na chini ya ukingo wake kulikuwa na mapambo ya vibuyu,^c nayo yalizunguka ukingo wote, vibuyu kumi kwa kila mkono mmoja kuzunguka Bahari yote, na safu mbili za vibuyu zilitengenezwa kwa kuyeyushwa zikiwa sehemu ya Bahari hiyo. 25 Ilikuwa juu ya ng'ombe dume 12,^d watatu wakitazama kaskazini, watatu wakitazama magharibi, watatu wakitazama kusini, na watatu wakitazama mashariki; na Bahari hiyo ilikuwa juu yao, na sehemu zao zote za nyuma zilielekea katikati. 26 Na unene wake ulikuwa upana wa kiganja kimoja;^{*} na ukingo wake ulitengenezwa kama ukingo wa kikombe, kama ua la yungiyungi. Ingeweza kujaa maji kiasi cha bathi 2,000.[#]

27 Kisha akatengeneza magari kumi^{*e} ya shaba. Kila gari lilikuwa na urefu wa mikono minne, upana wa mikono minne, na kimo cha mikono mitatu. 28 Na hivi ndivyo magari hayo yalivyotengenezwa: Yalikuwa na kuta za pembeni, na kuta hizo za pembeni zilikuwa kati ya mihimili. 29 Na

7:23 *Au "tangi." #Au "ilikuwa na mzingo wa mikono 30." 7:26 *Karibu sentimita 7.4 (inchi 2.9). Angalia Nyongeza B14. #Bathi ilikuwa sawa na lita 22. Angalia Nyongeza B14. 7:27 *Au "mikokoteni kumi ya maji."

kwenye kuta hizo za pembeni kati ya mihimili hiyo kulikuwa na simba,^a ng'ombe dume, na makerubi,^b na muundo huo-huo ulikuwa kwenye mihimili. Juu na chini ya simba na ng'ombe dume hao kulikuwa na mashada ya maua yaliyoyeyushwa. **30** Na kila gari lilikuwa na magurudumu manne ya shaba na vyuma vya katikati vya shaba vinavyozungusha magurudumu hayo, na nguzo nne za pembeni ziliyashikilia. Na kila upande chini ya beseni kulikuwa na vitegemezo vilivyotengenezwa kwa mashada ya maua yaliyoyeyushwa. **31** Mdomo wake ulikuwa katika sehemu ya juu, nao ulichomoza juu kwa kipimo cha mkono mmoja; na mdomo huo ulikuwa na mviringo, na kitako chote kilikuwa na urefu wa mkono mmoja na nusu, na mdomo wake ulikuwa na michongo. Na kuta za pembeni za magari hayo zilikuwa za mraba, si mviringo. **32** Na yale magurudumu manne yalikuwa chini ya kuta hizo, na nguzo zilizoshikilia magurudumu ziliungani-shwa na gari, na kila gurudumu lilikuwa na kimo cha mkono mmoja na nusu. **33** Na magurudumu hayo yalitengenezwa kama magurudumu ya gari la vita. Nguzo zake, mizingo yake, njukuti,* na vitovu vya magudurumu, vyote vilitengenezwa kwa kuyeyushwa. **34** Kulikuwa na nguzo nne kwenye pembe nne za kila gari; nguzo hizo zilitengenezwa kwa kuyeyushwa zikiwa sehemu ya gari hilo.* **35** Juu ya gari hilo kulikuwa na utepe

7:33 *Au "tindi." 7:34 *Au "zilikuwa kipande kimoja na gari hilo."

SURA YA 7

a Eze 41:19

b Mwa 3:24
Kut 25:18
1Fa 6:27
2Nya 3:7
Eze 41:17, 18

Safu ya 2

a 1Fa 6:29
1Fa 6:32

b 1Fa 7:27

c 1Fa 7:15, 46
2Nya 4:3

d Kut 30:18

e 2Nya 4:6, 10

f 1Fa 7:13
2Nya 2:13g Kut 27:3
2Fa 25:14

h Kut 24:6

i 2Nya 4:11-17

j 1Fa 7:15

k 1Fa 7:17

wa mviringo wenye kimo channusu mkono, na viunzi vyake na kuta zake za pembeni zilikuwa juu ya gari hilo, nazo zilitengenezwa kwa kuyeyushwa zikiwa sehemu ya gari hilo.* **36** Juu ya viunzi vyake na kwenye kuta zake za pembeni alichonga makerubi, simba, na mitende kulingana na nafasi iliyopatikana kwenye kila kipande, na mashada ya maua kuzunguka pande zote.^a **37** Hivyo ndivyo alivyoyatengeneza magari hayo kumi;^b yote yalitengenezwa kwa kuyeyushwa kwa njia ileile,^c yakiwa na vipimo na umbo lilelile.

38 Alitengeneza mabeseni kumi ya shaba;^d kila beseni lingeweza kujaa kiasi cha bathi 40 za maji. Kila beseni lilikuwa na upana wa mkono 4.* Kulikuwa na beseni moja kwa ajili ya kila majawapo ya magari hayo kumi. **39** Kisha akaweka magari matano upande wa kulia wa nyumba, na matano upande wa kushoto wa nyumba; akaiweka ile Bahari upande wa kulia wa nyumba, kuelekea kusini mashariki.^e

40 Hiramuf^f alitengeneza pia mabeseni, sepetu,^g na makabuli.^h

Basi Hiramu akamaliza kazi yote aliyomfanyia Mfalme Sulemani kuhusiana na nyumba ya Yehova:ⁱ **41** zile nguzo mbili^j na vifuniko vyenye umbo la bakuli vilivyo-kuwa juu ya nguzo hizo; na nyavu mbili^k za kufunika vifuniko hivyo viwili vyenye umbo la bakuli vilivyokuwa juu ya nguzo hizo; **42** yale

7:35 *Au "zikiwa kipande kimoja na gari hilo." 7:38 *Au "kipenyo cha mikono minne."

makomamanga 400^a kwa ajili ya zile nyavu mbili, safu mbili za makomamanga kwa ajili ya kila wavu, ili kufunika vile vifuniko viwili vyenye umbo la bakuli vilivyokuwa juu ya zile nguzo mbili; **43** yale magari kumi^b na yale mabeseni kumi^c yaliyokuwa juu ya magari hayo; **44** ile Bahari^d na wale ng'ombe dume 12 waliokuwa chini ya Bahari hiyo; **45** na ndoo za kuondolea majivu, sepetu, mabakuli, na vyombo vyote ambavyo Hiramu alimtengenezea Mfalme Sulemani kwa shaba iliyong'arishwa kwa ajili ya nyumba ya Yehova. **46** Mfalme alivitegemeza katika kalibu za udongo wa mfinyanzi katika wilaya ya Yordani, kati ya Sukothi na Sarethani.

47 Sulemani hakupima uzito wa chombo chochote kwa sababu vyombo hivyo vilikuwa vingi sana. Uzito wa shaba haukujulikana.^e **48** Sulemani alivitegemeza vitu vyote vya nyumba ya Yehova: madhabahu^f ya dhahabu; meza ya dhahabu^g ya kuwekea mikate ya wonyesho; **49** vinara vya taa^h vya dhahabu safi, vitano upande wa kulia na vitano upande wa kushoto mbele ya chumba cha ndani zaidi; na maua,ⁱ taa, na koleo, vyote vya dhahabu;^j **50** mabeseni, mikasi ya kukatia tamba za taa,^k mabakuli, vikombe,^l na vyetezo,^m vyote vya dhahabu safi; na bawaba za milango ya nyumba ya ndani,ⁿ yaani, Patakatifu Zaidi, na za milango ya nyumba ya hekalu,^o vyote vya dhahabu.

51 Kwa hiyo Mfalme Sulemani akakamilisha kazi yote aliyopaswa kufanya kwa ajili

SURA YA 7

a 1Fa 7:20

b 1Fa 7:27

c 1Fa 7:38

d 1Fa 7:23

e 1Nya 22:14, 16
2Nya 4:18-22

f Kut 37:25

g Kut 37:10

h Kut 37:17
Ufu 1:20

i 1Fa 6:18

j Kut 37:23

k Yer 52:18

l Kut 25:29

m Law 16:12

n 1Fa 6:31

o 1Fa 6:33

Safu ya 2

a 2Sa 8:10-12

b 2Nya 5:1

SURA YA 8

c Mhu 1:1

d 2Nya 5:2, 3

e 2Sa 6:17

f 2Sa 5:7
1Nya 11:5g Law 23:34
Kum 16:13h 1Nya 15:2, 15
2Nya 5:4-6i Kut 40:2
2Nya 1:13

j 1Nya 16:1

k Kut 26:33
Kut 40:21
2Sa 6:17
Ufu 11:19l 1Fa 6:27
2Nya 5:7
Zb 80:1
Eze 10:5

ya nyumba ya Yehova. Kisha Sulemani akaingiza ndani vitu ambavyo Daudi baba yake alikuwa amevifanya kuwa vitakatifu,^a naye akaweka fedha, dhahabu, na vitu hivyo katika hazina za nyumba ya Yehova.^b

8 Wakati huo Sulemani aliwakusanya^c wazee wa Israeli—viongozi wote wa makabila, wakuu wa koo* za Israeli.^d Wakaja kwa Mfalme Sulemani huko Yerusalemu ili kuliondoa sanduku la agano la Yehova katika Jiji la Daudi,^e yaani, Sayuni.^f **2** Wanaume wote wa Israeli wakakusanyika mbele ya Mfalme Sulemani wakati wa sherehe* katika mwezi wa Ethanimu,^g yaani, mwezi wa saba.^g **3** Basi wazee wote wa Israeli wakaja, na makuhani wakalibeba Sanduku.^h **4** Wakalipandisha kutoka huko Sanduku la Yehova, hema la mkutano,ⁱ na vyombo vyote vitakatifu vilivyokuwa katika hema hilo. Makuhani na Walawi wakavipandisha vitu hivyo. **5** Mfalme Sulemani na Waisraeli wote waliokusanywa ili wakutane naye, walikuwa mbele ya Sanduku. Kondoo na ng'ombe wengi sana wasiohesabika au kujulikana idadi walikuwa wakitolewa dhabihu.^j

6 Kisha makuhani wakalilita sanduku la agano la Yehova mahali pake,^k katika chumba cha ndani zaidi cha nyumba, yaani, Patakatifu Zaidi, chini ya mabawa ya makerubi.^l

7 Kwa hiyo mabawa ya makerubi yalikuwa yamenyoshwa juu ya mahali ambapo Sanduku liliwekwa, hivi kwa-

8:1 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

8:2 *Yaani, Sherehe ya Vibanda.

*Angalia Nyongeza B15.

mba makerubi hao walilifunika Sanduku na fito zake.^a **8** Fito hizo^b zilikuwa ndefu sana hivi kwamba ncha zake zilionekana kutoka Patakatiifu mbele ya chumba cha ndani zaidi, lakini hazikuonekana kutoka upande wa nje. Nazo ziko huko mpaka leo hii. **9** Hakukuwa na kitu kingine ndani ya Sanduku hilo isipokuwa yale mabamba mawili ya mawe^c ambayo Musa aliyaweka humo^d kule Horebu, Yehova alipofanya agano^e na Waisraeli walipokuwa wakitoka nchini Misri.^f

10 Makuhani walipotoka mahali patakatiifu, wingu^g lilijaa katika nyumba ya Yehova.^h **11** Makuhani hawakuweza kusimama ili kuhudumu kwa sababu ya wingu hilo, kwa maana utukufu wa Yehova ulijaa katika nyumba ya Yehova.ⁱ **12** Wakati huo Sulemani akasema: "Yehova alisema kwamba atakaa katika giza zito.^j **13** Nimefanikiwa kukujengea nyumba iliyo-kwezwa, mahali palipofanywa imara ili ukae humo milele."^k

14 Kisha mfalme akageuka na kuanza kulibariki kutaniko lote la Waisraeli huku kutaniko lote la Waisraeli likiwa limesimama.^l **15** Akasema: "Na asifiwe Yehova Mungu wa Israeli, ambaye kwa kinywa chake mwenyewe alimwahidi baba yangu Daudi, na kwa mkono wake mwenyewe ametimiza, akisema, **16** 'Kuanzia siku niliyowatoa watu wangu Waisraeli nchini Misri, sijachagua jiji katika makabila yote ya Israeli na kujenga humo nyumba ili jina langu likae humo,^m lakini nimemchagua Daudi awa-

SURA YA 8

a Kut 25:20
2Nya 5:8-10b Kut 25:14
Kut 37:4c Kum 4:13
Ebr 9:4d Kut 40:20
Kum 10:5

e Kut 24:8

f Kut 19:1
Hes 10:11, 12g Kut 40:34
Law 16:2

h 2Nya 5:11-14

i Kut 40:35
Eze 10:4
Eze 43:4
Eze 44:4
Mdo 7:55
Ufu 21:23j Kut 20:21
Kum 5:22
2Nya 6:1, 2
Zb 18:11
Zb 97:2k Zb 78:69
Zb 132:13, 14

l 2Nya 6:3-11

m Kum 12:11

Safu ya 2

a 2Sa 7:1-3
1Nya 17:1, 2

b 2Sa 7:12, 13

c 1Nya 28:5, 6

d Kut 34:28
Kum 9:9
Kum 31:26

e 2Nya 6:12

f Kut 15:11
1Sa 2:2
2Sa 7:22

g Kum 7:9

h 2Nya 6:14-17

tawale watu wangu Waisraeli.' **17** Moyo wa baba yangu Daudi ulitamani kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wa Israeli.^a **18** Lakini Yehova akamwambia Daudi baba yangu, 'Moyo wako ulitamani kujenga nyumba kwa ajili ya jina langu, na ulifanya vizuri kutamani jambo hilo moyoni mwako. **19** Hata hivyo, hutajenga nyumba hiyo, lakini mwana wako mwenyewe utakayemzaa* ndiye atakayejenga nyumba hiyo kwa ajili ya jina langu.'^b **20** Yehova ametimiza ahadi hiyo aliyoitoa, kwa maana nimechukua mahali pa baba yangu Daudi na kuketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli, kama Yehova alivyoahidi. Pia nimejenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wa Israeli,^c **21** nami nimetenga mahali humo kwa ajili ya lile Sanduku lenye agano^d ambalo Yehova alifanya na mababu zetu alipokuwa akiwatoa nchini Misri."

22 Kisha Sulemani akasimama mbele ya madhabahu ya Yehova mbele ya kutaniko lote la Waisraeli, akanyoosha mikono yake kuelekea mbinguni,^e **23** akasema: "Ee Yehova Mungu wa Israeli, hakuna Mungu kama wewe^f juu mbinguni wala chini duniani, unayeshika agano na kuwatandea kwa upendo mshikamanifu^g watumishi wako wanaotembea mbele zako kwa moyo wao wote.^h **24** Umetimiza ahadi uliyomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu. Ulitoa ahadi hiyo kwa kinywa chako mwenyewe, na siku ya leo umeitimiza kwa mkono wako

8:19 *Tnn., "mwana wako, atakayetoka katika viuno vyako."

mwenyewe.^a **25** Na sasa, Ee Yehova Mungu wa Israeli, timiza ahadi uliyomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu ulipomwambia, 'Hutakosa kamwe mwanamume wa uzao wako atakayeketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli mbele zangu, ikiwa tu wana wako watakazia uangalifu njia yao kwa kutembea mbele zangu, kama ulivyotembea mbele zangu.'^b **26** Na sasa, Ee Mungu wa Israeli, tafadhali acha ahadi uliyomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu ithibitike kuwa ya kweli.

27 "Lakini Ee Mungu, je, kweli utakaa duniani?^c Tazama! Mbingu, naam, mbingu za mbingu, haziwezi kukutoshia;^d sembuse nyumba hii nilioyijenga!^e **28** Sasa sikiliza sala yangu mimi mtumishi wako na ombi langu la kutaka kibali, Ee Yehova Mungu wangu, sikiliza kilio changu cha kuomba msaada na sala ambayo mimi mtumishi wako ninasali leo mbele zako. **29** Macho yako na yatazame nyumba hii usiku na mchana, yatazame mahali ambapo ulisema hivi kupahusu: 'Jina langu litakuwa hapo,'^f ili usikilize sala ambayo mimi mtumishi wako ninasali kuelekea mahali hapa.^g **30** Nawe usikilize ombi langu mimi mtumishi wako la kutaka kibali na pia ombi ambalo watu wako Waisraeli wanaomba kuelekea mahali hapa, nawe usikilize katika makao yako mbinguni;^h naam, usikilize na kusamehe.ⁱ

31 "Mwanadamu akimtendea dhambi mwanadamu mwenzake, naye aapishwe* na

8:31 *Au "aliyetendewa dhambi akimweka chini ya laana." Yaani, kiapo kinacholeta laana ikiwa mtu anaapa kwa uwongo au kukosa kutimiza kiapo hicho.

SURA YA 8

a 2Sa 7:12,13

b 1Fa 2:4
Zb 132:12

c Isa 66:1

d Zb 148:13
Yer 23:24e 2Nya 2:6
2Nya 6:18-21
Ne 9:6
Mdo 17:24f Kut 20:24
2Sa 7:13g Da 6:10
1Pe 3:12

h Zb 33:13

i 2Nya 7:13,14
Da 9:19

Safu ya 2

a 2Nya 6:22,23

b Ayu 34:11

c Law 26:14,17
Yos 7:8,11
2Fa 17:6,7

d Ne 1:11

e 2Fa 19:19,20
2Nya 6:24,25

f Zb 106:47

g Law 26:19
Kum 28:23

h Eze 14:13

i 2Nya 6:26,27

j Isa 30:20
Isa 54:13

k 1Fa 18:1

l Law 26:16
2Fa 6:25m Kum 28:21,22
Amo 4:9

kuwekwa chini ya wajibu wa kiapo hicho,* naye akiwa chini ya kiapo* aje mbele ya madhabahu yako katika nyumba hii,^a **32** basi usikie kutoka mbinguni na kuchukua hatua na kuwahukumu watumishi wako kwa kumtangaza yule mwovu kuwa na hatia na kumwadhibu kwa sababu ya jambo alilotenda,* na kumtangaza mwadilifu kuwa asiye na hatia^a na kumthawabisha kulingana na uadilifu wake mwenyewe.^b

33 "Watu wako Waisraeli wakishindwa na maadui kwa sababu ya kuzidi kukutendea dhambi,^c nao warudi kwako na kulitukuza jina lako^d na kusali na kukusihi wapate kibali katika nyumba hii,^e **34** basi usikie kutoka mbinguni na kuwasamehe watu wako Waisraeli dhambi yao na kuwarudisha katika nchi uliyowapa mababu zao.^f

35 "Mbingu zikifungwa ku siwe na mvua^g kwa sababu wamezidi kukutendea dhambi,^h nao wasali kuelekea mahali hapa na kulitukuza jina lako na kuacha dhambi yao kwa sababu umewanyenyekeza,ⁱ **36** basi usikie kutoka mbinguni na kuwasamehe watumishi wako dhambi yao, dhambi ya watu wako Waisraeli, kwa sababu utawafundisha/ njia nzuri wanayopaswa kufuata; na ulete mvua katika nchi yako^k ambayo uliwapa watu wako kuwa urithi.

37 "Njaa kali ikitokea nchini,^l au ugonjwa hatari, upepo unaochoma, kuvu,^m maku-

8:31 *Tnn., "laana." **8:32** *Tnn., "kuleta juu ya kichwa chake mwenyewe jambo alilotenda." # Tnn., "kuwa mwadilifu." **8:35** *Au "umewatesa."

ndi ya nzige, au parare* wanaokula sana; au maadui wao wakiwazingira katika jiji lolote nchini[#] au pigo au ugonjwa wa aina yoyote ukitokea,^a **38** sala yoyote, ombi lolote la kutaka kibali^b ambalo hueda likatolewa na mtu yeyote au na watu wako wote Waisraeli (kwa sababu kila mmoja anajua mateso yaliyo katika moyo wake mwenyewe)^c wakinyoosha mikono yao kuelekea nyumba hii, **39** basi usikie kutoka mbinguni, makao yako,^d nawe usamehe^e na kuchukua hatua; na umthawabishe kila mmoja kulingana na njia zake zote,^f kwa sababu unajua moyo wake (ni wewe peke yako unayejua vizuri moyo wa kila mwanadamu),^g **40** ili wakuogope siku-zote watakazoishi katika nchi uliyowapa mababu zetu.

41 "Pia mgeni ambaye si sehemu ya watu wako Waisraeli na ambaye anatoka katika nchi ya mbali kwa sababu ya jina lako*^h **42** (kwa maana watasikia kuhusu jina lako kuuⁱ na mkono wako wenye nguvu na mkono wako ulio-nyoosha), akija na kusali kuelekea nyumba hii, **43** basi usikilize kutoka mbinguni, makao yako,^j nawe ufanye mambo yote ambayo mgeni huyo anakuomba ufanye, ili watu wote duniani wajue jina lako na kukuogopa,^k kama watu wako Waisraeli wanavyokuogopa, na ili wajue kwamba nyumba hii niliyojenga imeitwa kwa jina lako.

44 "Watu wako wakienda vitani kupigana na maadui

SURA YA 8

a 2Nya 6:28-31

b 2Nya 33:12, 13

c Met 14:10

d Isa 63:15

e Zb 130:4

f Ayu 34:11

Zb 18:20

g 1Sa 16:7

1Nya 28:9

Yer 17:10

h Hes 9:14

Ru 1:16

2Fa 5:15

2Nya 6:32, 33

Isa 56:6, 7

Mdo 8:27

i Ne 9:10

j Zb 11:4

k Zb 67:2

Zb 102:15

Safu ya 2

a Kut 23:31

1Fa 20:13

b 2Nya 14:11

2Nya 20:5, 6

c Zb 78:68

Zb 132:13

d 2Nya 6:34, 35

e Zb 51:5

Zb 130:3

Mhu 7:20

Ro 3:23

1Yo 1:8

f Kum 28:15, 36

2Fa 17:6

2Fa 25:21

2Nya 6:36-39

g Law 26:40

h Kum 4:27, 29

Kum 30:1, 2

2Nya 33:12, 13

i Ne 1:6

Zb 106:6

Met 28:13

Da 9:5

j 1Sa 7:3

k Da 6:10

l Isa 63:15

m 2Nya 30:9

Ezr 7:28

Ne 2:7, 8

n Kut 19:5

Kum 9:26

o Kut 14:30

wao mahali utakapowaelekeza,^a nao wasali^b kwako wewe, Yehova, kuelekea jiji ambalo umechagua^c na kuelekea nyumba ambayo nimejenga kwa ajili ya jina lako,^d **45** basi usikie kutoka mbinguni sala yao na ombi lao la kutaka kibali, nawe utekeleze hukumu kwa ajili yao.

46 "Wakikutendea dhambi (kwa sababu hakuna mwanadamu asiyetenda dhambi),^e nawe uwakasirikie vikali na kuwaacha mikononi mwa maadui, na waliowateka wawapeleke katika nchi ya maadui, mbali au karibu;^f

47 nao warudiwe na ufa-hamu wakiwa katika nchi ya watu waliowachukua mateka,^g na kukurudia^h na kuomba kibali chako wakisema, "Tumetenda dhambi na kukosea; tumetenda uovu,"ⁱ **48** nao waturudie kwa moyo wao wote^j na kwa nafsi* yao yote katika nchi ya maadui wao waliowachukua mateka, nao wasali kwako kuelekea nchi yao ambayo uliwapa mababu zao na kuelekea jiji ambalo umelechagua na nyumba ambayo nimejenga kwa ajili ya jina lako,^k **49** basi usikie kutoka mbinguni, makao yako,^l sala yao na ombi lao la kutaka kibali, nawe utekeleze hukumu kwa ajili yao **50** na uwasamehe watu wako ambao wamekutendea dhambi, na kusamehe makosa yote waliyokukosea. Utafanya waliowateka wawahurumie,* nao watawahurumia^m **51** (kwa maana wao ni watu wako na urithi wako,ⁿ uliowatoa Misri,^o

8:37 *Au "panzi." [#]Tnn., "katika nchi ya malango yake." 8:41 *Au "sifa yako."

8:48 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 8:50 *Tnn., "Utawafanya wawe vitu vya kuhurumiwa mbele ya waliowateka."

kutoka ndani ya tanuru la kuyeyushia chuma).^a **52** Macho yako yatazame ombi langu mimi mtumishi wako la kutaka kibali^b na ombi la kutaka kibali la watu wako Waisraeli kwa kuwasikiliza wakati wowote wanapokulilia.*^c **53** Kwa maana uliwatenga wawe urithi wako kutoka kati ya mataifa yote ya dunia,^d kama ulivyotangaza kupitia mtumishi wako Musa ulipokuwa ukiwatoa mababu zetu Misri, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

54 Mara tu Sulemani alipomaliza kumtolea Yehova sala hiyo yote na kuomba kibali chake, aliinuka kutoka mbele ya madhabahu ya Yehova, mahali alipokuwa amepiga magoti akiwa amenyooша mikonoyake kuelekea mbinguni.^e **55** Kisha akasimama na kulibariki kwa sauti kubwa kutaniko lote la Waisraeli aki sema: **56** “Na asifiwe Yehova, ambaye amewapa watu wake Waisraeli mahali pa kupumzikia, kama alivyoahidi.^f Hakuna ahadi yoyote kati ya ahadi zake zote nzuri ambazo aliahidi kupitia Musa mtumishi wake iliyokosa kutimia.^g **57** Yehova Mungu wetu na awe pamoja nasi kama tu alivyokuwa pamoja na mababu zetu.^h Naye asituache wala kututupa.ⁱ **58** Na aivute moyo yetu kwake/ ili tutembe kati ka njia zake zote na kushika amri zake, masharti yake, na sheria zake,* ambazo aliwaamuru mababu zetu washike. **59** Na maneno haya yangu ambayo nimesema ili kumwo-

8:52 *Au “kuwasikiliza wanapokuomba jambo lolote.” **8:58** *Tnn., “maamuzi yake.”

SURA YA 8

a Kum 4:20

b 2Nya 6:40

c Zb 86:5
Zb 145:18d Kut 19:6
Kum 4:34
Kum 32:9

e 2Nya 6:12, 13

f 1Fa 4:24, 25

g Kum 10:11
Yos 21:45h Kum 31:6
Yos 1:5
2Nya 32:7
Zb 46:7i Isa 41:10
Ebr 13:5j Zb 86:11
Zb 119:36
2Th 3:5

Safu ya 2

a Yos 4:24
1Sa 17:46
Eze 36:23
Eze 39:7b Kum 4:35, 39
Isa 44:6c Kum 18:13
2Fa 20:3
1Nya 28:9
Mt 22:37

d 2Nya 7:4, 5

e Law 3:1

f Ezz 6:16
Ne 12:27

g 2Nya 4:1

h Law 3:16

i Law 23:34

j Mwa 15:18
Hes 34:5, 8

mba Yehova kibali na yawe karibu na Yehova Mungu wetu mchana na usiku, ili atekeze hukumu kwa ajili yangu mimi mtumishi wake na kwa ajili ya watu wake Waisraeli kulingana na mahitaji ya kila siku, **60** ili mataifa yote duniani yajue kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli.^a Hakuna mwingine!^b **61** Basi acheni moyo yenu iwe kamili^c kwa* Yehova Mungu wetu kwa kufuata masharti yake na kushika amri zake kama ilivyo leo.”

62 Kisha mfalme na Waisraeli wote wakamtolea Yehova dhabihu kubwa.^d **63** Sulemani alimtolea Yehova dhabihu za ushirika:^e Alitoa ng’ombe 22,000 na kondoo 120,000. Basi mfalme na Waisraeli wote wakaizindua nyumba ya Yehova.^f **64** Siku hiyo ilimbidi mfalme atakase sehemu ya katikati ya ua ulio mbele ya nyumba ya Yehova, kwa sababu alipaswa kutolea mahali hapo dhabihu za kutekelezwa, matoleo ya nafaka, na vipande vya mafuta vya dhabihu za ushirika, kwa sababu madhabahu ya shaba^g iliyo mbele za Yehova ilikuwa ndogo sana isiweze kutoshea dhabihu za kutekelezwa, matoleo ya nafaka, na vipande vya mafuta^h vya dhabihu za ushirika. **65** Wakati huo Sulemani alifanya sherehe hiyoⁱ pamoja na Waisraeli wote, kutaniko kubwa kuanzia Lebo-hamathi* na kushuka mpaka kwenye Korongo[†] la Misri,^j mbele za Yehova Mungu wetu kwa siku 7 na kisha siku nyingine 7, jumla ya

8:61 *Au “imtumikie kikamili.” **8:65** *Au “njia ya kuingia Hamathi.” [†]Angalia Kamusi, uku. 2012.

siku 14. **66** Siku iliyofuata,* aliwaruhusu watu waondoke, nao wakambariki mfalme na kwenda nyumbani kwao wakashangilia na kufurahi moyoni kwa sababu ya wema wote.^a ambao Yehova alikuwa amemtendea Daudi mtumishi wake na watu wake Waisraeli.

9 Mara tu Sulemani alipomaliza kujenga nyumba ya Yehova, nyumba ya mfalme,^{*b} na kila kitu ambacho Sulemani alitamani kufanya,^c **2** Yehova akamtokea Sulemani mara ya pili, kama alivyokuwa amemtokea kule Gibeoni.^d **3** Yehova akamwambia: “Nimesikia sala yako na ombi lako la kutaka kibali ulilotoa mbele zangu. Nimeitakasa nyumba hii ambayo umejenga kwa kuliweka jina langu humu milele,^e na macho yangu na moyo wangu utakuwa humu sikuzote.^f **4** Nawe, ikiwa utatembea mbele zangu kama Daudi baba yako alivyotembea,^g kwa utimilifu wa moyo^h na kwa unyoofu,ⁱ kwa kutenda mambo yote niliyokuamuru,^j nawe ukitii masharti yangu na sheria* zangu,^k **5** ndipo nitakapoirarisha kiti chako cha ufalme juu ya Israeli milele, kama nilivyomwahidi Daudi baba yako, kwa ku-sema, ‘Hutakosa kamwe mwanamume wa uzao wako atakayeketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli.’^l **6** Lakini ikiwa ninyi na wana wenu mtageuka na kuacha kunifuata na kuacha kushika amri zangu na maagizo yangu ambayo nime-weka mbele yenu, nanyi mwe-

8:66 *Tnn., “Siku ya nane,” yaani, siku iliyofuata kipindi cha pili cha siku saba. **9:1** *Au “jumba la mfalme.” **9:4** *Tnn., “hukumu.”

SURA YA 8

a Zb 31:19
Isa 63:7
Yer 31:12

SURA YA 9

b 2Nya 8:1
Mhu 2:4

c 2Nya 7:11

d 1Fa 3:5

e Kum 12:5, 6
1Fa 8:28, 29

f 2Nya 6:40
2Nya 16:9
Zb 132:13

g 1Fa 3:6

h Zb 78:70, 72

i 1Nya 29:17

j Mhu 12:13

k 2Nya 7:17, 18

l 2Sa 7:16, 17
1Fa 2:4
Zb 89:20, 29

Safu ya 2

a 1Fa 11:4
2Nya 7:19-22

b Law 18:28
Kum 4:26
2Sa 7:14
2Fa 17:22, 23
Zb 89:30-32

c 2Fa 25:9, 10
2Nya 15:2

d Kum 28:37
Zb 44:14

e 2Nya 36:19
Isa 64:11

f Kum 29:24, 25
Yer 22:8, 9

g Kum 28:64
Yer 5:19
Yer 12:7

h 1Fa 6:37-7:1
2Nya 8:1, 2

i 1Fa 5:1, 7

j 1Fa 5:8

nde na kuabudu miungu mingine na kuiinamia.^a **7** nita-waondolea mbali Waisraeli kutoka katika nchi ambayo nime-wapa,^b na nyumba ambayo nimeitakasa kwa ajili ya jina langu nitaitupilia mbali kutoka mbele za macho yangu,^c na Israeli itakuwa kitu cha kudharauliwa* na kitu cha kudhihakiwa miongoni mwa mataifa yote.^d **8** Na nyumba hii itakuwa marundo ya magofu.^e Kila mtu atakayepita karibu nayo ataitazama kwa mshangao, atapiga mluzi na kuuliza, ‘Kwa nini Yehova alite-ndea hivi nchi hii na nyumba hii?’^f **9** Kisha watasema, ‘Ni kwa sababu walimwacha Yehova Mungu wao, aliyewatoa mababu zao kutoka nchini Misri, nao wakashikamana na miungu mingine, wakaiinamia na kuiabudu. Ndiyo sababu Yehova aliwaletea msiba huo wote.’^g

10 Katika muda wa miaka 20 ambayo Sulemani alijenga nyumba hizo mbili, yaani, nyumba ya Yehova na nyumba ya* mfalme,^h **11** Hiramⁱ mfalme wa Tiro alimpa Sulemani mbao za mierezi na mbao za miberoshi na dhahabu nyingi sana kadiri alivyohitaji,^j naye Mfalme Sulemani akampa Hiram majiji 20 katika nchi ya Galilaya. **12** Basi Hiram akatoka Tiro kwenda kuyao-na majiji ambayo Sulemani alikuwa amempa, lakini hakuridhika nayo.* **13** Akamuuliza: “Ndugu yangu, ni majiji gani haya ambayo umenipa?” Basi tangu siku hiyo yakaitwa Nchi

9:7 *Tnn., “methali.” **9:10** *Au “jumba la.” **9:12** *Tnn., “hayakuwa sawa machoni pake.”

ya Kabuli.* **14** Wakati huo, Hiram akamtumia mfalme talanta 120* za dhahabu.^a

15 Habari ifuatayo inawahusu watu ambao Mfalme Sulemani aliwaandikisha kufanya kazi ya kulazimishwa^b ili wajenge nyumba ya Yehova,^c nyumba yake mwenyewe,* Kilima,^{#d} ukuta wa Yerusalemu, Hasori,^e Megido,^f na Gezeri.^g

16 (Farao mfalme wa Misri alikuwa amekuwa na kuliteka jiji la Gezeri na kulitekteza kwa moto, na alikuwa pia amewaua Wakanaan^h walioishi katika jiji hilo. Basi akampa binti yake,ⁱ mke wa Sulemani, jiji hilo kama zawadi ya kumuaga.*) **17** Sulemani akalijenga* jiji la Gezeri, Bethoron la Chini,^j **18** Baalathi,^k na Tamari lililo nyikani, yaliyokuwa nchini, **19** na pia majiji yote ya Sulemani yenye maghala, majiji ya magari ya vita,^l majiji ya wapanda farasi, na chochote ambacho Sulemani alitamani kujenga huko Yerusalemu, Lebanoni, na katika nchi yote iliyokuwa chini ya mamlaka yake. **20** Watu wengine wote waliobaki miongoni mwa Waamori, Wahiti, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi,^m ambao hawakuwa sehemu ya taifa la Israeli,ⁿ **21** wazao wao waliobaki nchini, ambao Waisraeli walishindwa kuwaangamiza, Sulemani aliwaandikisha ili wafanye kazi ya kulazimishwa

9:13 *Au labda, "Nchi lisiyofaa Kitu."

9:14 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

9:15 *Au "jumba lake mwenyewe la mfalme." 9:15, 24 *Au "Milo." Neno la Kiebrania linaloanishwa "jaza." 9:16

*Au "zawadi ya harusi; mahari." 9:17 *Au "akaliimarisha."

SURA YA 9

a 1Fa 10:21

b 1Fa 4:6
1Fa 5:13

c 1Fa 6:37

d 2Sa 5:9
1Fa 11:27
2Fa 12:20

e Yos 19:32, 36

f Yos 17:11
Amu 5:19
2Fa 9:27

g Amu 1:29

h Yos 16:10

i 1Fa 3:1

j Yos 16:1, 3
2Nya 8:4-6

k Yos 19:44, 48

l 1Fa 4:26

m Hes 13:29
Kum 7:1
Amu 1:21

n 2Nya 8:7-10

Safu ya 2

a Mwa 9:25

b Law 25:39

c 1Fa 5:16
2Nya 2:18

d 1Fa 3:1
1Fa 7:8
2Nya 8:11

e 2Sa 5:9

f 1Fa 9:15

g Kut 23:14

h 2Nya 8:12, 13

i 2Nya 8:16

j Kum 2:8

k 2Nya 8:17, 18

l 1Fa 5:12

m Mwa 10:29
1Nya 29:3, 4
Zb 45:9

SURA YA 10

n 1Fa 4:29

o 2Nya 9:1, 2
Mt 12:42

kama watumwa mpaka leo hii.^a **22** Lakini Sulemani hakumfanya Mwisraeli yeyote kuwa mtumwa,^b kwa sababu walikuwa mashujaa wake, watumishi, wakuu, makamanda wasaidizi, wakuu wa wale walioendesha magari yake ya vita na wapanda farasi wake.

23 Kulikuwa na wakuu 550 wa wasaidizi waliosimamia kazi ya Sulemani, wasimamizi wa watu waliokuwa wakifanya kazi.^c

24 Lakini binti ya Farao^d akatoka katika Jiji la Daudi^e akaenda kuishi katika nyumba yake ambayo Sulemani alimjengea; kisha Sulemani akajenga Kilima.^{#f}

25 Mara tatu kwa mwaka^g Sulemani alitoa dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za ushirika kwenye madhabahu aliyomjengea Yehova,^h pia alifukiza moshi wa dhabihu kwenye madhabahu iliyokuwa mbele za Yehova, basi akaikamilisha nyumba.ⁱ

26 Mfalme Sulemani akategeneza pia kundi la meli katika jiji la Esion-geberi,^j lililo kando ya Elothi, ufuoni mwa Bahari Nyekundu katika nchi ya Edomu.^k **27** Hiram akawatuma watumishi wake mwenyewe, mabaharia wenye uzoefu, wakafanye kazi pamoja na watumishi wa Sulemani kwenye kundi hilo la meli.^l **28** Wakaenda Ofiri,^m wachukua talanta 420 za dhahabu na kumletea Mfalme Sulemani.

10 Basi malkia wa Sheba alisikia habari za Sulemani kuhusiana na jina la Yehova,ⁿ kwa hiyo akaja kumjaribu kwa maswali magumu.*^o

10:1 *Au "mafumbo."

2 Alifika Yerusalemu na msafara wenye kuvutia sana,^a pamoja na ngamia waliobeba mafuta ya zeri^b na dhahabu nyingi sana na mawe yenye thamani. Akafika mbele ya Sulemani na kumwambia mambo yote yaliyokuwa moyoni mwake. **3** Kisha Sulemani akajibu maswali yake yote. Hakuna jambo lolote lililokuwa gumu sana* kwa mfalme asiweze kumweleza.

4 Malkia wa Sheba alipona hekima yote ya Sulemani,^c nyumba aliyojenga,^d

5 chakula kilichokuwa meza ni pake,^e jinsi watumishi wake walivyoketi, jinsi watumishi wake walivyohudumu meza ni na pia mavazi yao, na wale waliompa vinywaji, na dhahabu zake za kuteketezwa alizotoa kwa ukawaida katika nyumba ya Yehova, alipigwa na bumbuzi.* **6** Basi akamwambia mfalme: “Habari nilizosikia katika nchi yangu kuhusu mafanikio* yako na kuhusu hekima yako zilikuwa za kweli. **7** Lakini sikuamini habari hizo mpaka nilipokuja na kujiona kwa macho yangu mwenyewe. Na kwa kweli sikuwa nimeambiwa hata nusu yake. Hekima yako na ufanisi wako umezidi kwa mbali habari nilizosikia. **8** Wenye furaha ni watu wako, na wenye furaha ni watumishi wako wanaosimama mbele yako daima, wakiisikiliza hekima yako!^f **9** Na asifiwe Yehova Mungu wako,^g ambaye amependezwa nawe, akakuweka kwenye kiti cha ufalme cha Israeli. Kwa sababu ya upendo wa milele

10:3 *Tnn., “lililofichwa.” 10:5 *Tnn., “hakubaki na roho yoyote ndani yake.” 10:6 *Au “maneno.”

SURA YA 10

a Zb 72:10

b Kut 25:3, 6
2Fa 20:13

c 1Fa 3:28
Mhu 12:9

d 2Nya 9:3-8

e 1Fa 4:22

f Met 8:34

g 1Fa 5:7

Safu ya 2

a Mwa 43:11

b Zb 72:10

c 1Fa 9:27, 28
Zb 45:9

d 2Nya 2:8

e 2Nya 9:10, 11

f 2Nya 5:12
Zb 150:3

g 2Nya 9:12

h 2Nya 9:13, 14

wa Yehova kwa Waisraeli, alikuweka rasmi kuwa mfalme ili utekeleze haki na uadilifu.”

10 Kisha akampa mfalme talanta 120* za dhahabu na kiasi kikubwa sana cha mafuta ya zeri^a na mawe yenye thamani.^b Mfalme Sulemani hakuwahi tena kuletewa kiasi kikubwa hivyo cha mafuta ya zeri kama alicholetewa na malkia wa Sheba.

11 Kundi la meli za Hiram zilizobeba dhahabu kutoka Ofiri^c zilileta pia mbao nyingi sana za misandali kutoka Ofiri,^d na mawe yenye thamani.^e **12** Mfalme alitumia mbao hizo za misandali kutengeneza vitegemezi vya nyumba ya Yehova na nyumba ya mfalme,* na pia vinubi na vinanda vya waimbaji.^f Mbao za misandali kama hizo hazijawahi tena kuletwa wala kuonekana mpaka leo hii.

13 Mfalme Sulemani alimpa pia malkia wa Sheba kitu chochote alichotamani na kuomba, mbali na vitu alivyompa kwa ukarimu wake mwenyewe.* Baada ya hayo aliondoka na kurudi katika nchi yake, pamoja na watumishi wake.^g

14 Na dhahabu iliyoletwa kwa Sulemani katika mwaka mmoja ilikuwa na uzito wa talanta 666 za dhahabu,^h **15** mbali na dhahabu iliyoletwa na wafanyabiashara wasafiri na pia faida kutoka kwa wauzaji wa bidhaa na kutoka kwa wafalme wote wa Uarabuni na magavana wa nchi.

10:10 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. 10:12 *Au “jumba la mfalme.” 10:13 *Tnn., “kulingana na mkono wa Mfalme Sulemani.”

16 Mfalme Sulemani alitengeneza ngao kubwa **200** za dhahabu iliyochanganywa na madini mengine^a (kwa kila ngao alitumia shekeli **600*** za dhahabu)^b **17** na ngao ndogo* **300** za dhahabu iliyochanganywa na madini mengine (kwa kila ngao ndogo alitumia mina tatu^c za dhahabu). Kisha mfalme akaziweka katika Nyumba ya Msitu wa Lebanoni.^c

18 Mfalme pia alitengeneza kiti kikubwa cha ufalme cha pembe za tembo^d na kufunika kwa dhahabu safi.^e

19 Kiti hicho cha ufalme kilikuwa na ngazi sita, kilikuwa na kifuniko cha mviringo mgongoni, nacho kilikuwa na mikono pande zote mbili, na simba wawili^f walisimama kando ya mikono hiyo. **20** Na kulikuwa na simba **12** waliosimama kwenye ngazi hizo sita, wawili kwenye kila ngazi, mmoja upande huu na mwingine upande wa pili. Hakuna ufalme mwingine wowote uliokuwa umetengeneza kiti kama hicho.

21 Vyombo vyote vya kunywea vya Mfalme Sulemani vilikuwa vya dhahabu, na vyombo vyote vya Nyumba ya Msitu wa Lebanoni^g vilikuwa vya dhahabu safi. Hakukuwa na kitu chochote kilichotengenezwa kwa fedha, kwa maana fedha ilionwa kuwa si kitu katika siku za Sulemani.^h **22** Mfalme alikuwa na kundi la meli za Tarshishiⁱ baharini pamoja na kundi la meli za

10:16 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. **10:17** *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale. ^cKatika Maandiko ya Kiebrania mina moja inalingana na gramu 570. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 10

a 1Fa 14:25, 26

b 2Nya 9:15, 16

c 1Fa 7:2

d Zb 122:2, 5

e 2Nya 9:17-19

f Mwa 49:9
Hes 23:24
Hes 24:9

g 1Fa 7:2

h 2Nya 9:20, 21

i Mwa 10:4
Zb 72:10
Eze 27:12
Yon 1:3

Safu ya 2

a 1Fa 10:18

b Mhu 5:19

c 1Fa 3:12, 13
1Fa 4:29
2Nya 9:22-24

d Met 2:6

e Kum 17:15, 16
1Fa 4:26f 2Nya 1:14
2Nya 9:25g 2Nya 1:15
2Nya 9:27h 2Nya 1:16, 17
2Nya 9:28

i Yos 1:4

Hiramu. Mara moja baada ya kila miaka mitatu, kundi la meli za Tarshishi zilikuja zikiwa zimejazwa dhahabu na fedha, pembe za tembo,^a sokwe, na tausi.

23 Kwa hiyo Mfalme Sulemani alikuwa na utajiri^b mwingi zaidi na hekima^c kuliko wafalme wengine wote duniani. **24** Na watu wote duniani walitaka kukutana na* Sulemani ili wasikie hekima yake ambayo Mungu alikuwa ameweka moyoni mwake.^d **25** Kila mmoja wao alileta zawadi—vitu vya fedha, vitu vya dhahabu, mavazi, silaha, mafuta ya zeri, farasi, na nyumba—na walifanya hivyo mwaka baada ya mwaka.

26 Na Sulemani akaendelea kukusanya magari ya vita na farasi;* akawa na magari **1,400** ya vita na farasi* **12,000,**^e naye aliwaweka katika majiji ya magari ya vita karibu naye huko Yerusalemu.^f

27 Mfalme alifanya fedha huko Yerusalemu iwe nyingi kama mawe, na mbao za mie-rezi ziwe nyingi kama mikuyu katika Shefela.^g

28 Farasi wa Sulemani waliletwa kutoka Misri, na wafanyabiashara wa mfalme walinunua makundi ya farasi* kwa bei moja.^h **29** Kila gari kutoka Misri lilinunuliwa kwa vipande **600** vya fedha, na farasi alinunuliwa kwa vipande **150**; kisha waliwauzia wafalme wote wa Wahitiⁱ na wafalme wa Siria.

10:24 *Tnn., "waliutafuta uso wa." **10:26** *Au "wapanda farasi." **10:28** *Au labda, "kutoka Misri na kutoka Kue; wafanyabiashara wa mfalme waliwanunua kutoka Kue," huenda ni Kilikia.

11 Lakini mbali na binti ya Farao,^a Mfalme Sulemani aliwapenda wanawake wengi wa kigeni:^b wanawake Wa-moabu,^c Waamoni,^d Waedomu, Wasidoni,^e na Wahiti.^f **2** Walitoka katika mataifa ambayo Yehova alikuwa amewambia hivi Waisraeli kuyahusu: "Hampaswi kuingia miongoni mwao,* nao hawapaswi kuingia miongoni mwenu; kwa maana kwa hakika wataigeuza mioyo yenu ifuate miungu yao."^g Lakini Sulemani alishikamana nao na kuwapenda. **3** Naye alikuwa na wake 700 waliokuwa mabinti wa wafalme na masuria 300, na hatua kwa hatua wake zake wakaugeuza moyo wake.* **4** Sulemani alipozeeka,^h wake zake waliugeuza* moyo wake ukiafuata miungu mingine,ⁱ na moyo wake haukuwa kamili kwa[#] Yehova Mungu wake kama moyo wa Daudi baba yake. **5** Na Sulemani akamfuata Ashtorethi,^j mungu wa kike wa Wasidoni, na Milkomu,^k mungu mwenye kuchukiza wa Waamoni. **6** Na Sulemani akatenda maovu machoni pa Yehova, naye hakumfuata Yehova kikamili kama Daudi baba yake alivyomfuata.^l

7 Wakati huo ndipo Sulemani alipojenga mahali pa juu^m kwa ajili ya Kemoshi, mungu mwenye kuchukiza wa Moabu, kwenye mlima uliokuwa mbele ya Yerusalemu, na kwa ajili ya Moleki,ⁿ mungu mwenye kuchukiza wa Waamoni.^o **8** Hivyo ndivyo alivyowafanyia wake zake wote

11:2 *Au "Hampaswi kuoana nao." 11:3 *Au "wake zake wakawa na uvutano mkubwa kwake." 11:4 *Au "waliupotosha." #Au "haukumtumikia kikamili."

SURA YA 11

a 1Fa 3:1

b Kum 17:15, 17
Ne 13:26

c Mwa 19:36, 37

d 1Fa 14:21

e 1Fa 16:30, 31

f Mwa 26:34, 35

g Kut 34:16
Kum 7:3
Yos 23:12, 13
2Ko 6:14

h 1Fa 11:42

i Kum 7:3, 4
Ne 13:26j Amu 2:11, 13
Amu 10:6
1Sa 7:3

k Sef 1:5

l 1Fa 15:5

m Law 26:30
Hes 33:52
2Fa 21:1, 3n Law 18:21
Mdo 7:43

o 2Fa 23:13

Safu ya 2

a Kum 7:3, 4
Met 4:23b 1Fa 3:5
1Fa 9:2

c 2Nya 7:19, 20

d 2Fa 17:21

e 2Nya 10:18, 19

f 2Sa 7:12, 15

g 1Fa 12:20
2Nya 11:1

h Kum 12:11

i 2Sa 7:12, 14

j Mwa 27:40

k 2Sa 8:13

wa kigeni waliokuwa wakifukiza moshi wa dhabihu na kuitolea dhabihu miungu yao.

9 Yehova akamkasirikia vikali Sulemani, kwa sababu moyo wake ulikuwa umegeuka na kumwacha Yehova Mungu wa Israeli,^a aliyekuwa amemtokea mara mbili^b **10** na kumwonya kuhusu jambo hilo-hilo, kwamba hapaswi kuifua miungu mingine.^c Lakini hakutii amri ya Yehova.

11 Sasa Yehova akamwambia Sulemani: "Kwa sababu ume-fanya jambo hili, nawe hukushika agano langu na sheria zangu nilizokuamuru, kwa hakika nitaurarua ufalme kutoka kwako, nami nitampa mmoja wa watumishi wako.^d **12** Hata hivyo, kwa ajili ya Daudi baba yako, sitafanya hivyo maishani mwako. Nitaurarua kutoka mikononi mwa mwana wako,^e **13** lakini sitaurarua ufalme wote.^f Kabila moja nitampa mwana wako,^g kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu na kwa ajili ya Yerusalemu, jiji ambalo nimechagua."^h

14 Ndipo Yehova akatokeza mtu wa kumpinga Sulemani,ⁱ yaani, Hadadi Mwedomu, wa ukoo wa kifalme wa Edomu.^j

15 Daudi aliposhinda Edomu,^k Yoabu mkuu wa jeshi alipanda kwenda kuwazika waliouawa, naye akajaribu kumuua kila mwanamume huko Edomu.

16 (Kwa maana Yoabu na Waisraeli wote walikaa huko kwa miezi sita mpaka alipokuwa amemwangamiza kila mwana-mume huko Edomu.) **17** Lakini Hadadi alikimbia pamoja na baadhi ya Waedomu waliokuwa watumishi wa baba yake, wakaenda Misri; wakati

huo Hadadi alikuwa mvulana mdogo. **18** Basi wakaondoka Midiani na kufika Parani. Wali-chukua wanaume kutoka Parani^a na kwenda Misri, kwa Farao mfalme wa Misri, ambaye alimpa nyumba, akaamuru awe akipewa chakula, na pia akampa ardhi. **19** Hadadi alipata kibali machoni pa Farao, hivi kwamba akampa dada ya mke wake mwenyewe, dada ya malkia Tapenesi,* ili amwoe. **20** Baada ya muda dada ya Tapenesi akamzalia mwana, Genubathi, na Tapenesi alimlelea* katika nyumba ya Farao; Genubathi aliendelea kukaa katika nyumba ya Farao miongoni mwa wana wa Farao.

21 Hadadi akasikia akiwa Misri kwamba Daudi alikuwa amekufa na kuzikwa pamoja na mababu zake^b na kwamba Yoabu mkuu wa jeshi alikuwa amekufa.^c Basi Hadadi akamwambia Farao: "Niruhusu niende zangu, niende katika ardhi yangu mwenyewe."

22 Lakini Farao akamuuliza: "Ni nini ulichokosa kwangu hivi kwamba unataka kwenda katika ardhi yako mwenyewe?" Hadadi akamjibu: "Sijakosa chochote, lakini tafadhali niruhusu niende zangu."

23 Mungu akatokeza pia mtu mwingine wa kumpinga Sulemani,^d yaani, Rezonni mwana wa Eliada, aliyekuwa amemkimbia bwana wake, Hadadezeri^e mfalme wa Soba. **24** Alijikusanyia wanaume akawa kiongozi wa kundi la wavamizi wakati Daudi alipowashinda.*^f Basi wakaeenda Damasko,^g wakakaa huko

11:19 *Hakuwa malkia aliyetawala.
11:20 *Au labda, "alimwachisha kunyonya."
11:24 *Tnn., "alipowaua."

SURA YA 11

a Hes 10:12

b 1Fa 2:10

c 1Fa 2:34

d 1Fa 11:14

e 2Sa 8:3

f 2Sa 10:18

g 2Sa 8:5
1Fa 19:15
Isa 7:8

Safu ya 2

a 1Fa 11:31
1Fa 12:32
1Fa 14:10
2Nya 11:14
2Nya 13:3, 20

b 1Fa 9:22

c 2Nya 13:6

d 1Fa 9:15, 24

e 2Sa 5:7

f 1Fa 5:16

g 1Fa 12:15
1Fa 14:2
2Nya 9:29

h 1Fa 12:16

i 1Fa 12:20
2Nya 11:1

j Mwa 49:10

na kuanza kutawala huko Damasko. **25** Naye akawa mpinzani wa Waisraeli siku zote za Sulemani, kuongezea madhara yaliyosababishwa na Hadadi, naye aliwachukua sana Waisraeli alipokuwa akitawala Siria.

26 Pia kulikuwa na Yero-boamu^a mwana wa Nebati, Mwefraimu kutoka Sereda, mtumishi wa Sulemani,^b na mama yake aliyekuwa mjane aliitwa Serua. Yeye pia alianza kumwasi* mfalme.^c **27** Hii ndiyo sababu iliyomfanya amwasi mfalme: Sulemani alikuwa amejenga Kilima*^d na kuziba mwanya katika ukuta wa Jiji la Daudi baba yake.^e

28 Sasa huyu Yeroboamu alikuwa mwanamume mwenye uwezo mkubwa. Sulemani alipoona kwamba kijana huyo alikuwa mfanyakazi mwenye bidii, alimweka kuwa msimamizi^f wa utumishi wote wa lazima wa nyumba ya Yosefu. **29** Wakati huo Yeroboamu alitoka Yerusalemu, na nabii Ahiya,^g Mshilo, akamkuta njiani. Ahiya alikuwa amevaa nguo mpya, na wote wawili walikuwa peke yao shambani.

30 Ahiya akashika nguo mpya aliyokuwa amevaa na kuirarua vipande 12. **31** Kisha akamwambia Yeroboamu:

"Jichukulie vipande kumi, kwa maana Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: 'Tazama, ninaurua ufalme kutoka mikononi mwa Sulemani, nami nitakupa makabila kumi.^h

32 Lakini atabaki na kabila mojaⁱ kwa ajili ya mtumishi wangu Daudi^j na kwa ajili ya

11:26 *Tnn., "kuinua mkono wake dhidi ya." 11:27 *Au "Milo." Neno la Kiebrania linalomaanisha "jaza."

Yerusalemu, jiji ambalo nimechagua miongoni mwa makabila yote ya Israeli.^a **33** Nitafanya hivyo kwa sababu wame-niacha,^b nao wanamwinamia Ashtorethi, mungu wa kike wa Wasidoni, na Kemoshi, mungu wa Moabu, na Milkomu, mungu wa Waamoni, nao hawajatembea katika njia zangu kwa kufanya yaliyo sawa machoni pangu na kushika maagizo yangu na sheria zangu* kama Daudi baba yake alivyofanya. **34** Lakini sitaachukua ufalme wote kutoka mikononi mwake, nami nitamwacha aendelee kuwa mkuu sikuzote za maisha yake, kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu niliyemchagua,^c kwa sababu alitii amri zangu na sheria zangu. **35** Lakini nitau-chukua ufalme kutoka mikononi mwa mwana wake na kukupa wewe, yaani, makabila kumi.^d **36** Nitampa mwana wake kabila moja, ili sikuzote Daudi mtumishi wangu awe na taa mbele zangu Yerusalemu,^e jiji ambalo nimejichagulia liwe mahali pa kuweka jina langu. **37** Nitakuchukua wewe, nawe utatawala kila kitu unachotamani,* nawe utakuwa mfalme wa Israeli. **38** Na ikiwa utatii mambo yote ninayokuamuru na kutembea katika njia zangu na kufanya yaliyo sawa machoni pangu kwa kutii sheria zangu na amri zangu, kama Daudi mtumishi wangu alivyofanya,^f nitakuwa pia pamoja nawe. Nitakujengea nyumba inayodumu, kama nilivyomjengea Daudi,^g nami nitakupa Israeli. **39** Nami nitauaibisha

11:33 *Tnn., "maamuzi yangu." 11:37

*Au "ambacho nafsi yako inatamani."

SURA YA 11

a Kum 12:5, 6
1Fa 11:13
Zb 132:13

b Kum 28:15
2Nya 15:2

c 1Fa 9:4, 5
Zb 89:49
Zb 132:17
Isa 9:7

d 1Fa 12:20
2Nya 10:16

e 2Sa 7:29
1Fa 15:4
2Fa 8:19

f 1Fa 15:5

g 2Sa 7:11

Safu ya 2

a 1Fa 12:16

b Mwa 49:10
Isa 11:1
Lu 1:32, 33

c 1Fa 14:25

d 2Nya 10:2

e 2Nya 9:29-31

f 1Nya 3:10
2Nya 13:7
Mt 1:7

SURA YA 12

g Mwa 12:6
Yos 20:7, 9
Amu 9:1, 2
Mdo 7:15, 16

h 2Nya 10:1-4

i 1Fa 11:26, 40

j 1Sa 8:11-18
1Fa 4:7

k 2Nya 10:5-7

uzao wa Daudi kwa sababu ya jambo hili,^a lakini sitafanya hivyo sikuzote."^b

40 Basi Sulemani akajari-bu kumuua Yeroboamu, lakini Yeroboamu akakimbilia Misri, kwa Mfalme Shishaki^c wa Misri,^d akaendelea kukaa Misri mpaka Sulemani alipokufa.

41 Na mambo mengine katika historia ya Sulemani, mambo yote aliyofanya na hekima yake, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya Sulemani?^e **42** Sulemani alitawala nchi yote ya Israeli kwa miaka 40 akiwa Yerusalemu. **43** Kisha Sulemani akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi baba yake; na Rehoboamu^f mwanawe akawa mfalme baada yake.

12 Rehoboamu alienda Shekemu, kwa maana Waisraeli wote walikuwa wamekujia Shekemu^g kumfanya kuwa mfalme.^h **2** Mara tu Yeroboamu mwana wa Nebati aliposikia habari hizo (bado alikuwa akiishi Misri kwa sababu alikuwa amemkimbia Mfalme Sulemani),ⁱ **3** wakawatuma watu waende kumwita. Kisha Yeroboamu na Waisraeli wote wakaja kwa Rehoboamu na kumwambia hivi: **4** "Baba yako aliifanya nira yetu kuwa nzito.^j Lakini ukiufanya utumishi mzito wa baba yako kuwa mwepesi zaidi na kupunguza nira nzito* aliyotutwika, tutakutumikia."

5 Ndipo akawaambia: "Nendeni, kisha mrudi baada ya siku tatu." Basi watu wakae-nda zao.^k **6** Kisha Mfalme Rehoboamu akashauriana na

12:4 *Au "inayokandamiza."

wanaume wazee waliomtumikia Sulemani baba yake alipokuwa hai, akawauliza: “Mnani-shauri niwape jibu gani watu hawa?” **7** Wakamjibu: “Leo ukiwa mtumishi wa watu hawa na kukubali ombi lao na kuwapa jibu linalofaa, watakuwa watumishi wako sikuzote.”

8 Hata hivyo, alikataa ushauri aliopewa na wanaume wazee, akashauriana na vijana wa rika lake na ambao sasa walikuwa watumishi wake.^a **9** Aliwauliza: “Mnashauri tuwape jibu gani watu hawa ambao wameniambia, ‘Ifanye nira ambayo baba yako alitutwika iwe nyepesi zaidi?’” **10** Vijana hao wa rika lake wakamwambia: “Hivi ndivyo unavyopaswa kuwaambia watu hao waliokwambia, ‘Baba yako aliifanya nira yetu kuwa nzito, lakini wewe unapaswa kuifanya kuwa nyepesi zaidi kwa ajili yetu’; hivi ndivyo unavyopaswa kuwaambia, ‘Kidole changu kidogo kitakuwa kinene kuliko kiuno cha baba yangu. **11** Baba yangu aliwatwika nira nzito, lakini mimi nitazidisha uzito wa nira yenu. Baba yangu aliwaadhibu kwa mijeledi, lakini mimi nitawaadhibu kwa mijeledi yene miiba.”

12 Yeroboamu na watu wote wakaja kwa Rehoboamu siku ya tatu, kama mfalme alivyokuwa amesema: “Rudini kwangu siku ya tatu.”^b **13** Lakini mfalme akawajibu watu kwa ukali, akaukataa ushauri aliopewa na wanaume wazee. **14** Akawajibu kama alivyoshauriwa na vijana wa rika lake, na kusema: “Baba yangu aliifanya nira yenu kuwa nzito, lakini mimi nitazidisha uzito

SURA YA 12

a 2Nya 10:8-11

b 2Nya 10:12-15

Safu ya 2

a Kum 2:30
2Nya 22:7
Ro 9:18

b 1Fa 11:31

c 2Nya 10:16, 17

d 1Fa 11:12, 13
2Nya 11:13, 16e 2Sa 20:24
1Fa 4:6
1Fa 5:13, 14

f 2Nya 10:18, 19

g 2Fa 17:21

h 1Fa 11:30, 31

i 1Fa 11:12, 13
Ho 11:12

wa nira yenu. Baba yangu aliwaadhibu kwa mijeledi, lakini mimi nitawaadhibu kwa mijeledi yenye miiba.” **15** Basi mfalme hakuwasikiliza watu, kwa sababu Yehova ndiye aliyesababisha badiliko hilo la mambo,^a ili atimize neno ambalo Yehova alimwambia Yeroboamu mwana wa Nebati kupitia Ahiya^b Mshilo.

16 Waisraeli wote walipooona kwamba mfalme amekataa kuwasikiliza, wakamwambia hivi mfalme: “Tuna ushirika gani na Daudi? Hatuna urithi wowote katika mwana wa Yese. Nendeni kwa miungu yenu, enyi Waisraeli! Sasa itunze nyumba yako mwenyewe, Ee Daudi!” Ndipo Waisraeli wakarudi katika nyumba zao.*^c **17** Lakini Rehoboamu akaendelea kuwatawala Waisraeli walioishi katika majiji ya Yuda.^d

18 Kisha Mfalme Rehoboamu akamtuma Adoramu,^e aliyekuwa msimamizi wa watu waliofanya kazi ya kulazimishwa, lakini Waisraeli wote wakamuua kwa kumpiga mawe. Mfalme Rehoboamu akafaulu kupanda gari lake na kukimbilia Yerusalemu.^f **19** Na tangu siku hiyo Waisraeli wamekuwa wakiasi^g nyumba ya Daudi.

20 Mara tu Waisraeli wote waliposikia kwamba Yeroboamu amerudi, wakamwita mbele ya kusanyiko, nao wakamweka kuwa mfalme wa Waisraeli wote.^h Hakuna yeyote aliyefuata nyumba ya Daudi isipokuwa kabila la Yuda.ⁱ

21 Rehoboamu alipofika Yerusalemu, mara moja ali-

12:16 *Tnn., “mahema yao.”

ikusanya nyumba yote ya Yuda na kabila la Benjamini, mashujaa 180,000 waliozozwa,* ili wapigane na nyumba ya Israeli na kuurudisha ufalme kwa Rehoboamu mwana wa Sulemani.^a **22** Kisha neno hili la Mungu wa kweli likamjia Shemaya^b mtu wa Mungu wa kweli: **23** “Mwambie Rehoboamu mwana wa Sulemani mfalme wa Yuda na nyumba yote ya Yuda na Benjamini na watu wengine, **24** ‘Hivi ndivyo Yehova anavyosema: “Msipande kwenda kupigana na ndugu zenu Waisraeli. Kila mmoja wenu anapaswa kurudi nyumbani kwake, kwa maana nimesababisha mambo haya yatukie.””^c Basi wakaliti neno la Yehova na kurudi nyumbani, kama Yehova alivyo waambia.

25 Kisha Yeroboamu akalijenga* jiji la Shekemu^d katika eneo lenye milima la Efraimu na kuishi humo. Kutoka huko, akaenda kulijenga^e jiji la Penueli.^e **26** Yeroboamu akasema moyoni mwake: “Sasa ufalme utarudi katika nyumba ya Daudi.^f **27** Watu hawa wakiendelea kupanda kwenda kutoa dhabihu katika nyumba ya Yehova huko Yerusalemu,^g mioyo ya watu hawa itamrudia pia bwana wao, Mfalme Rehoboamu wa Yuda. Naam, wataniau na kumrudia Mfalme Rehoboamu wa Yuda.” **28** Baada ya kushauriana, mfalme akatengeneza ndama wawili wa dhahabu^h na kuwambia watu: “Inachosha sana kwenu kupanda kwenda Yerusalemu. Ndiye huyu hapa

12:21 *Tnn., “waliochaguliwa.” 12:25 *Au “akaliimarisha.” #Au “kuliimarisha.”

SURA YA 12

a 2Nya 11:1-4
2Nya 25:5

b 2Nya 12:5

c 1Fa 11:30, 31

d 1Fa 12:1

e Mwa 32:30
Amu 8:13, 17

f 1Fa 11:38

g Kum 12:5, 6

h Kut 20:4
2Fa 10:29

Safu ya 2

a Kut 32:4, 8
2Nya 11:15, 16

b Mwa 12:8, 9
Mwa 28:19

c Mwa 14:14
Kum 34:1
Amu 18:29
Amu 20:1

d 2Fa 10:31
2Fa 17:21-23

e Hes 3:10
1Fa 13:33
2Nya 11:14
2Nya 13:9

f Law 23:34

g Amo 7:13

SURA YA 13

h 2Fa 23:16, 17

i 1Fa 12:32
Amo 3:14

j 2Fa 21:24
2Fa 22:1

Mungu wenu, enyi Waisraeli, aliyewatoa nchini Misri.”^a **29** Kisha akamweka ndama mmoja kule Betheli,^b na mwingine akamweka kule Dani.^c **30** Na jambo hilo likawafanya watende dhambi,^d watu wa-kaenda mpaka Dani kuabudu ndama aliyekuwa huko.

31 Naye akajenga nyumba za ibada mahali pa juu na kuchagua makuhani kutoka miongoni mwa watu wa kawaida, ambao hawakuwa Walawi.^e **32** Pia, Yeroboamu akaanza-sha sherehe katika mwezi wa nane, siku ya 15 ya mwezi huo, kama ile sherehe iliyokuwa ikifanywa kule Yuda.^f Kwenye madhabahu aliojenga kule Betheli,^g alitoa dhabihu kwa wale ndama aliokuwa ametengeneza, na huko Betheli akaweka makuhani wahudumu mahali pa juu alipokuwa amejenga. **33** Katika siku ya 15 ya mwezi wa nane, mwezi aliojichagulia, akaanza kutoa dhabihu kwenye madhabahu aliyokuwa amejenga huko Betheli; akaanza sherehe kwa ajili ya Waisraeli, naye akapanda juu ya madhabahu ili kutoa dhabihu na kufukiza moshi wa dhabihu.

13 Kwa neno la Yehova, mtu fulani wa Mungu^h alikuja Betheli kutoka Yuda wakati Yeroboamu alipokuwa amesimama karibu na madhabahuⁱ ili kufukiza moshi wa dhabihu. **2** Kisha kwa neno la Yehova akapaza sauti dhidi ya madhabahu hiyo na kusema: “Ee madhabahu, madhabahu! Hivi ndivyo Yehova anavyosema, ‘Tazama! Mwana anayelitwa Yosia,^j atazaliwa katika nyumba ya Daudi!

Na juu yako atawatoa dhahabu makuhani wa mahali pa juu, wanaofukiza moshi wa dhahabu juu yako, naye atateketeza mifupa ya wanadamu juu yako.”^a **3** Akatoa ishara* siku hiyo, akisema: “Hii ndiyo ishara* ambayo Yehova ametangaza: Tazama! Madhabahu itapasuka, na majivu” yaliyo juu yake yatamwagika.”

4 Mara tu mfalme aliposikia neno ambalo mtu wa Mungu wa kweli alikuwa amesema dhidi ya madhabahu huko Betheli, Yeroboamu akanyoosha mkono wake kutoka kwenye madhabahu na kusema: “Mkamateni!”^b Mara moja mkono aliokuwa amemnyooshea ukakauka,* naye hakuweza kuurudisha nyuma.^c **5** Kisha madhabahu ikapasuka na majivu yakamwagika kutoka kwenye madhabahu kulingana na ile ishara* ambayo mtu wa Mungu wa kweli alitoka kwa neno la Yehova.

6 Sasa mfalme akamwambia mtu wa Mungu wa kweli: “Tafadhali, niombe kibali kutoka kwa* Yehova Mungu wako, na usali kwa ajili yangu ili nirudishiwe mkono wangu.”^d Ndipo yule mtu wa Mungu wa kweli akaomba kibali kutoka kwa Yehova, na mkono wa mfalme ukarudi kama ulivyokuwa mwanzoni. **7** Kisha mfalme akamwambia mtu wa Mungu wa kweli: “Twende nyumbani ukale chakula, nami nitakupa zawadi.” **8** Lakini mtu wa Mungu wa kweli akamwambia mfalme: “Hata ukinipa

13:3, 5 *Au “alama.” 13:3 #Au “majivu yenye mafuta,” yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhahabu. 13:4 *Au “ukapooza.” 13:6 *Au “utilize uso wa.”

SURA YA 13

a 2Fa 23:15, 16
2Nya 34:33b 2Nya 16:10
Yer 20:2

c 2Fa 6:18

d Kut 10:16, 17
Hes 21:7
Yer 37:3
Mdo 8:24

Safu ya 2

a 1Fa 13:1

nusu ya nyumba yako, siwezi kwenda pamoja nawe na kula mkate au kunywa maji mahali hapa. **9** Kwa maana hivi ndivyo nilivyoamriwa kwa neno la Yehova: ‘Hupaswi kula mkate wala kunywa maji, nawe hupaswi kurudi kwa kutumia njia uliyopitia ulipokuja hapa.’” **10** Basi akaondoka kupitia njia nyingine, naye hakurudi kwa kutumia njia aliyopitia alipokuja Betheli.

11 Kulikuwa na nabii fulani mzee aliyekaa Betheli, wanawe wakaja nyumbani na kumsimulia mambo yote ambayo mtu wa Mungu wa kweli alikuwa amefanya siku hiyo kule Betheli na maneno aliyomwambia mfalme. Baada ya kumsimulia baba yao mambo hayo, **12** baba yao akawauliza: “Alipitia njia gani?” Kwa hiyo wanawe wakamwonyesha njia aliyopitia mtu huyo wa Mungu wa kweli aliyetoka Yuda. **13** Sasa akawaambia wanawe: “Niwekeeni matandiko juu ya punda.” Basi wakamwekea matandiko juu ya punda, naye akapanda juu yake.

14 Akamfuata mtu wa Mungu wa kweli na kumkuta ameketi chini ya mti mkubwa. Kisha akamuuliza: “Je, wewe ndiye yule mtu wa Mungu wa kweli aliyetoka Yuda?”^a Akajibu: “Ni mimi.” **15** Akamwambia: “Twende nyumbani ukale mkate.” **16** Lakini akasema: “Siwezi kurudi pamoja nawe wala kukubali mwaliko wako, nami siwezi kula mkate wala kunywa maji pamoja nawe mahali hapa. **17** Kwa maana niliambiwa kwa neno la Yehova, ‘Hupaswi kula mkate wala kunywa maji huko. Hupaswi kurudi kupitia njia

uliyotumia kuja.” **18** Ndipo akamwambia: “Mimi pia ni nabii kama wewe, na malaika alinambia hivi kwa neno la Yehova: ‘Mwambie arudi pamoja nawe nyumbani kwako ili ale mkate na kunywa maji.’” (Alimtanganya.) **19** Basi akarudi pamoja naye ili ale mkate na kunywa maji nyumbani kwake.

20 Walipokuwa wameketi mezani, neno la Yehova likamjia nabii aliyekuwa amemrudisha, **21** naye akamwambia kwa sauti yule mtu wa Mungu wa kweli aliyetoka Yuda: “Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu uliasi agizo la Yehova, nawe hukushika amri ambayo Yehova Mungu wako alikupa, **22** lakini ulirudi kula mkate na kunywa maji mahali ambapo uliambiwa, “Usile mkate wala kunywa maji,” maiti yako haitazikwa katika makaburi ya mababu zako.’”^a

23 Baada ya mtu wa Mungu wa kweli kula mkate na kunywa maji, nabii mzee akaweka matandiko juu ya punda kwa ajili ya nabii aliyekuwa amemrudisha. **24** Kisha akaenda zake, lakini simba akakutana naye barabarani na kumuua.^b Maiti yake ikatupwa barabarani, na punda akasimama kando yake; simba pia alikuwa amesimama kando ya maiti hiyo. **25** Watu waliokuwa wakipita hapo waliona maiti hiyo ikiwa imetupwa barabarani na simba akiwa amesimama kando yake. Wakaenda na kusimulia habari hizo katika jiji ambamo yule nabii mzee alikuwa akiishi.

26 Nabii huyo aliyekuwa amemrudisha njiani aliposikia habari hizo, mara moja aka-

SURA YA 13

a 1Fa 13:30
2Fa 23:17, 18

b 2Sa 6:7
1Fa 20:35, 36
2Fa 17:25

Safu ya 2

a 1Fa 13:9

b 1Fa 13:21, 22

c 2Fa 23:17, 18

d Law 26:30
1Fa 12:29, 31

e 2Fa 23:15, 19

f 1Fa 12:25, 31

sema: “Ni yule mtu wa Mungu wa kweli aliyeeasi agizo la Yehova;^a kwa hiyo Yehova alimkabidhi kwa simba, amrarue na kumuua, kulingana na neno la Yehova alilokuwa amemwambia.”^b **27** Kisha akawaambia hivi wanawe: “Niwekeeni matandiko juu ya punda.” Basi wakaweka matandiko juu yake. **28** Halafu akaenda zake na kuikuta ile maiti imetupwa barabarani, punda na simba wakiwa wamesimama kando ya maiti hiyo. Simba hakuwa ameila maiti, wala hakuwa amemraru punda. **29** Nabii huyo mzee akaibeba maiti ya mtu wa Mungu wa kweli na kuweka juu ya punda, akairudisha katika jiji lake mwenyewe ili kumwombolezea na kumzika. **30** Basi akailaza maiti hiyo katika kaburi lake mwenyewe, nao wakaendelea kumlilia kwa sauti wakisema: “Ole wako, ndugu yangu!” **31** Baada ya kumzika, akawaambia wanawe: “Nitakapokufa, nizikeni mahali ambapo mtu wa Mungu wa kweli amezikwa. Ilazeni mifupa yangu kando ya mifupa yake.”^c **32** Neno la Yehova alilokuwa ametangaza dhidi ya madhabu iliyoko Betheli na dhidi ya nyumba zote za ibada zilizo mahali pa juu^d katika majiji ya Samaria hakika litatimia.”^e

33 Hata baada ya mambo hayo kutendeka, Yeroboamu hakuacha njia yake mbaya, lakini aliendelea kuchagua makuhani kutoka miongoni mwa watu wa kawaida ili wahudumu mahali pa juu.^f Alimweka kuwa kuhani* mtu yeyote

13:33 * Tnn., “Aliujaza mkono wa.”

aliyetaka kuwa kuhani, aki-sema: “Na awe mmoja wa ma-kuhuni wa mahali pa juu.”^a

34 Dhambi hiyo ya nyumba ya Yeroboamu^b ilisababisha waharibiwa na kuangamizwa kutoka duniani.^c

14 Wakati huo Abiya mwana wa Yeroboamu akawa mgonjwa. **2** Kwa hiyo Yeroboamu akamwambia mke wake: “Tafadhali, inuka, badili sura yako ili watu wasitambue kwamba wewe ni mke wa Yeroboamu, halafu uende Shilo. Tazama! Nabii Ahiya yuko huko. Yeye ndiye aliyesema kwamba mimi nitakuwa mfalme wa watu hawa.”^d **3** Chukua mikate kumi, keki zilizonyunyiziwa kitu, na chupa ya asali, uende kwake. Kisha atakwambia kitakachomkata mvulana huyu.”

4 Mke wa Yeroboamu akafanya mambo aliyoiambiwa na Yeroboamu. Akainuka na kwenda Shilo,^e akafika katika nyumba ya Ahiya. Ahiya alikodoa macho yake mbele, lakini hakuweza kuona kwa sababu ya umri wake.

5 Hata hivyo, Yehova alikuwa amemwambia Ahiya: “Tazama, mke wa Yeroboamu anakuja kutafuta habari kuhusu mwanawe, kwa sababu ni mgonjwa. Nitakwambia mambo utakayomwambia.* Atakapofika ataficha sura yake ili asijulikane.”

6 Mara tu Ahiya aliposikia sauti ya miguu ya mwanamke huyo alipokuwa akija mlangoni, akasema: “Ingia ndani, mke wa Yeroboamu. Kwa nini unaficha sura yako usijulikane? Nimeagizwa nikupe

14:5 *Au “Utamwambia hivi na hivi.”

SURA YA 13

a 2Nya 11:14, 15

b 1Fa 16:30, 31
2Fa 3:1, 3
2Fa 10:31
2Fa 13:1, 2

c 1Fa 14:10
1Fa 15:25-29
2Fa 17:22, 23

SURA YA 14

d 1Fa 11:30, 31

e Yos 18:1
1Sa 4:3

Safu ya 2

a 1Fa 11:30, 31
1Fa 12:20

b 1Fa 12:16

c 1Fa 15:5
Mdo 13:22

d Kum 27:15
2Nya 11:15

e Ne 9:26
Zb 50:17

f 1Fa 15:25-29

ujumbe mkali. **7** Nenda, ukamwambie Yeroboamu, ‘Hivi ndivyo anavyosema Yehova Mungu wa Israeli: “Nilikuinua kutoka miongoni mwa watu wako na kukufanya kuwa kiongozi wa watu wangu Waisraeli.”^a **8** Kisha nikaurarua ufalme kutoka katika nyumba ya Daudi na kukupa wewe.^b Lakini hujawa kama mtumishi wangu Daudi, ambaye alishika amri zangu na kunifuata kwa moyo wake wote, akite nda tu yaliyokuwa sawa machoni pangu.”^c **9** Lakini ume-tenda mambo mabaya zaidi kuliko wote waliokutangulia, nawe ulijitengenezea mungu mwingine na sanamu za chuma* ili kunikasirisha,^d mimi ndiye uliyenigeuzia mgongo.^e **10** Kwa sababu hiyo ninailetea msiba nyumba ya Yeroboamu, nami nitamwangamiza kila mwanamume* wa Yeroboamu, kutia ndani wasio na uwezo na walio dhaifu katika Israeli, nami nitaiifagia kabisa nyumba ya Yeroboamu,^f kama mtu anavyoondoa kabisa mavi mpaka yote yanapokwisha! **11** Mtu yeyote wa Yeroboamu atakayefia jijini, ataliwa na mbwa; na yeyote atakayefia shambani, ataliwa na ndege wa angani, kwa sababu Yehova amesema hayo.”

12 “Sasa inuka; nenda nyumbani kwako. Utakapotia mguu wako jijini, mtoto huyo atakufa. **13** Waisraeli wote watamwombolezea na kumzika, kwa maana ni yeye peke yake katika familia ya Yeroboamu atakayezikwa kaburini,

14:9 *Au “sanamu za kuyeyushwa.” **14:10** *Tnn., “mtu yeyote anayekojoa ukutani.” Huu ni msemu wa Kiebrania wa kuwadhara wanaume.

kwa sababu ni yeye tu katika nyumba ya Yeroboamu ambaye Yehova Mungu wa Israeli amepata jambo fulani jema ndani yake. **14** Yehova atajii-nulia mfalme wa Israeli atakayeiangamiza nyumba ya Yeroboamu^a kuanzia siku hiyo na kuendelea, naam, hata sasa. **15** Yehova atawapiga Waisraeli kama tete linaloyumba-yumba ndani ya maji, naye atawang'oa Waisraeli kutoka katika nchi hii nzuri aliyowapa mababu zao^b na kuwatawanya ng'ambo ya Mto Efrati,^c kwa sababu walimkasirisha Yehova kwa kutengeneza miti mitakatifu.*^d **16** Naye atawaacha Waisraeli kwa sababu ya dhambi ambazo Yeroboamu alitenda na kusababisha Waisraeli kuzitenda."^e

17 Basi mke wa Yeroboamu akainuka na kwenda zake, akafika Tirsu. Alipokaribia kizingiti cha mlango, mvulana huyo akafa. **18** Kwa hiyo wakamzika, na Waisraeli wote wakamwombolezea, kama Yehova alivyokuwa amesema kupitia nabii Ahiya, mtumishi wake.

19 Na mambo mengine katika historia ya Yeroboamu, jinsi alivyopigana vita^f na jinsi alivyotawala, yameandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli. **20** Yeroboamu alitawala kwa miaka 22, kisha akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake;^g na Nadabu mwanawe akawa mfalme baada yake.^h

21 Wakati huo, Rehoboamu mwana wa Sulemani alikuwa mfalme wa Yuda. Rehoboamu alikuwa na umri wa miaka 41

SURA YA 14

a 1Fa 15:25-29

b Kum 8:7-9
Kum 29:28
Yos 23:15
2Fa 17:6c Kum 28:64
2Fa 15:29
2Fa 18:11

d Kum 12:3

e 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33, 34f 2Nya 12:15
2Nya 13:3

g 2Nya 13:20

h 1Fa 15:25

Safu ya 2

a Zb 78:68
Zb 132:13b Kut 20:24
Kum 12:5, 6
1Fa 8:16, 17c 1Fa 11:1
2Nya 12:13d 1Fa 11:7
2Nya 12:1

e Isa 65:2

f Law 26:1

g Isa 65:7

h Kum 12:2, 3
Isa 57:5
Yer 2:20
Ho 4:13i Kum 23:17, 18
1Fa 15:11, 12
1Fa 22:46
2Fa 23:7
Ho 4:14

j 1Fa 11:40

k 2Nya 12:2-4

l 1Fa 7:51
1Fa 15:18
2Fa 18:14, 15
2Fa 24:12, 13m 1Fa 10:16, 17
2Nya 12:9-11

alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 17 huko Yerusalemu, jiji ambalo Yehova alichagua^a miongoni mwa makabila yote ya Israeli ili kuweka jina lake humo.^b Mama ya Rehoboamu alitwa Naama, naye alikuwa Mwamoni.^c **22** Na watu wa Yuda walikuwa wakitenda maovu machoni pa Yehova,^d na kwa dhambi zao walimkasirisha kuliko walivyofanya mababu zao.^e **23** Pia waliendelea kujijengea mahali pa juu, nguzo takatifu, na miti mitakatifu*^f juu ya kila kilima kirefu^g na chini ya kila mti wenye majani mengi.^h **24** Kulikuwa pia na wanaume makahaba wa hekaluni katika nchi.ⁱ Watu walitenda mambo yote yenye kuchukiza yaliyofanywa na mataifa ambayo Yehova alikuwa ameyafukuza kutoka mbele ya Waisraeli.

25 Katika mwaka wa tano wa Mfalme Rehoboamu, Mfalme Shishaki^j wa Misri alishambulia Yerusalemu.^k **26** Akachukua hazina za nyumba ya Yehova na hazina za nyumba ya mfalme.*^l Alichukua kila kitu, kutia ndani ngao zote za dhahabu ambazo Sulemani alikuwa ametengeneza.^m **27** Basi Mfalme Rehoboamu akatengeneza ngao za shaba zichukue mahali pa ngao hizo, akaziweka chini ya ulinzi wa mkuu wa walinzi,*ⁿ aliyelinda mlango wa nyumba ya mfalme. **28** Wakati wowote ambapo mfalme alikuja katika nyumba ya Yehova, walinzi walizichukua, kisha walizirudisha katika chumba cha walinzi.

29 Na mambo mengine katika historia ya Rehoboamu,

14:26 *Au "jumba la mfalme." 14:27 *Tnn., "wakimbaji."

mambo yote aliyofanya, je, hayaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda?^a **30** Kulikuwa na vita daima kati ya Rehoboamu na Yeroboamu.^b **31** Kisha Rehoboamu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.^c Mama yake aliitwa Naama, naye alikuwa Mwamoni.^d Na Abiyamu* mwana wake^e akawa mfalme baada yake.

15 Katika mwaka wa 18 wa utawala wa Mfalme Yeroboamu^f mwana wa Nebati, Abiyamu akawa mfalme wa Yuda.^g **2** Alitawala kwa miaka mitatu huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Maaka,^h mjukuu wa Abishalomu. **3** Aliendelea kutembea katika dhambi zote ambazo baba yake alitenda kabla yake, na moyo wake haukuwa kamili kwa* Yehova Mungu wake kama moyo wa Daudi babu yake. **4** Hata hivyo, kwa sababu ya Daudi,ⁱ Yehova Mungu wake alimpa taa huko Yerusalemu^j kwa kumwinua mwana wake atawale baada yake na kufanya jiji la Yerusalemu lidumu. **5** Kwa maana Daudi alitenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova, naye haku-geuka na kuacha jambo lolote ambalo Yeye alikuwa amewamuru sikuzote za maisha yake, isipokuwa kuhusiana na kisa cha Uria, Mhiti.^k **6** Na kulikuwa na vita kati ya Rehoboamu na Yeroboamu sikuzote za maisha yake.^l

7 Na mambo mengine katika historia ya Abiyamu, mambo yote aliyofanya, je, ha-

14:31 *Anaitwa pia Abiya. **15:3** *Au "haukumtumikia kikamili."

SURA YA 14

a 1Nya 27:24

2Nya 12:15

b 1Fa 15:6

c 1Fa 11:43

d 1Fa 11:1

2Nya 12:13

e 1Nya 3:10

Mt 1:7

SURA YA 15

f 1Fa 12:20

g 2Nya 13:1, 2

h 2Nya 11:20-22

i 2Sa 7:8, 12

Zb 89:33-37

Isa 37:35

Yer 33:20, 21

j 1Fa 11:36

2Nya 21:7

Zb 132:13, 17

k 2Sa 11:4, 15

Zb 51:Uta

l 1Fa 14:30

2Nya 12:15

Safu ya 2

a 2Nya 13:22

b 2Nya 13:3

c 1Nya 3:10

Mt 1:7

d 2Nya 14:1

e 2Nya 11:21, 22

f 2Nya 14:2-5

2Nya 14:11

2Nya 15:17

g Kum 23:17, 18

1Fa 14:24

1Fa 22:45, 46

h 1Fa 11:7

1Fa 14:22, 23

i 2Nya 11:18, 20

j Kum 7:5

2Fa 18:1, 4

2Nya 34:1, 4

k 2Sa 15:23

2Nya 15:16-18

Yoh 18:1

l Hes 33:52

Kum 12:2

1Fa 22:41, 43

m 1Nya 26:26, 27

n 1Fa 16:3, 12

yajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda?^a Kulikuwa pia na vita kati ya Abiyamu na Yeroboamu.^b **8** Kisha Abiyamu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi; na Asa mwanawe^c akawa mfalme baada yake.^d

9 Katika mwaka wa 20 wa Mfalme Yeroboamu wa Israeli, Asa alianza kutawala Yuda.

10 Alitawala Yerusalemu kwa miaka 41. Nyanya yake aliitwa Maaka,^e mjukuu wa Abishalomu. **11** Asa alitenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova,^f kama Daudi babu yake.

12 Aliwafukuza wanaume makahaba wa hekaluni kutoka nchini^g na kuondoa sanamu zote zenye kuchukiza* ambazo mababu zake walikuwa wametengeneza.^h **13** Hata alimwondoa Maakaⁱ nyanya yake kutoka katika cheo chake cha mama malkia, kwa sababu alikuwa ametengeneza sanamu chafu sana* kwa ajili ya ibada ya mti mtakatifu.[#] Asa akai-katakata sanamu hiyo chafu sana^j na kuiteketeza katika Bonde la Kidroni.^k **14** Lakini mahali pa juu hapakuondolewa.^l Hata hivyo, moyo wa Asa ulikuwa kamili kwa* Yehova maisha yake yote.[#] **15** Naye alileta katika nyumba ya Yehova vitu ambavyo yeye na baba yake walikuwa wamevifanya kuwa vitakatifu—fedha, dhahabu, na vyombo mbalimbali.^m

16 Kulikuwa na vita daima kati ya Asa na Baashaⁿ mfalme

15:12 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno "mavi," nalo hutumiwa kuonyesha dharau. **15:13** *Yaani, kingono. [#]Angalia Kamusi, uku. 2012. **15:14** *Au "ulimtumikia kikamili." [#]Tnn., "siku zake zote."

wa Israeli. **17** Basi Mfalme Baasha wa Israeli alikuja kushambulia Yuda, akaanza kujenga* Rama^a ili kumzuia mtu yeyote asitoke wala kuingia kwa* Mfalme Asa wa Yuda.^b **18** Ndipo Asa akachukua fedha yote na dhahabu iliyokuwa imebaki katika hazina za nyumba ya Yehova na hazina za nyumba ya* mfalme na kuwapa watumishi wake. Kisha Mfalme Asa akawatuma kwa Ben-hadadi mwana wa Tabrimoni mwana wa Hezioni, mfalme wa Siria,^c aliyekuwa akiishi Damasko, akamwambia: **19** "Kuna mkataba* kati yangu na wewe na kati ya baba yangu na baba yako. Ninakutumia zawadi ya fedha na dhahabu. Njoo, vunja mkataba wako[#] na Mfalme Baasha wa Israeli, ili aondoke kwangu." **20** Ben-hadadi akamsikiliza Mfalme Asa, akawatumia wakuu wa majeshi yake kushambulia majiji ya Israeli, wakashinda Iyoni,^d Dani,^e Abel-beth-maaka, eneo lote la Kinerethi, na nchi yote ya Naftali. **21** Baasha aliposikia habari hizo, mara moja akaacha kujenga* Rama, akaendelea kuishi Tirsas.^f **22** Kisha Mfalme Asa akawaita watu wote wa Yuda—hakuna aliyeachwa—nao wakabeba mawe na mbao zilizokuwa zikitumiwa na Baasha kujenga Rama, Mfalme Asa akazitumia kujenga* Geba^g kule Benjamini, na pia Mispa.^h

23 Na mambo mengine kati ka historia ya Asa, ukuu wake

15:17, 21, 22 *Au "kuimarisha; kujenga upya." 15:17 #Au "asiondoke wala kuingia katika eneo la." 15:18 *Au "jumba la." 15:19 *Au "agano." #Au "agano lako."

SURA YA 15

a Yos 18:21, 25

b 2Nya 16:1-6

c 2Nya 16:7

d 2Fa 15:29

e Amu 18:29
1Fa 12:28, 29f 1Fa 14:17
Wim 6:4

g Yos 21:8, 17

h Yos 18:21, 26
Amu 20:1
1Sa 7:5
Yer 40:6

Safu ya 2

a 2Nya 16:11-14

b 1Fa 22:42
2Nya 17:3, 4
2Nya 18:1
2Nya 19:4
Mt 1:8

c 1Fa 14:20

d 1Fa 14:7, 9

e 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33f Yos 19:44, 48
Yos 21:20, 23
1Fa 16:15

g 1Fa 14:9, 10

wote na mambo yote aliyofanya na majiji aliyojenga,* je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? Lakini alipozeeka alishikwa na ugonjwa miguuni.^a **24** Kisha Asa akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Dau-di babu yake; na Yehoshafati^b mwanawe akawa mfalme baada yake.

25 Nadabu^c mwana wa Yeroboamu akawa mfalme wa Israeli katika mwaka wa pili wa Mfalme Asa wa Yuda, naye alitawala Israeli kwa miaka miwili. **26** Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova na kufuata njia ya baba yake^d na dhambi yake aliyo-sababisha Waisraeli kutenda.^e

27 Baasha mwana wa Ahiya wa nyumba ya Isakari akapanga njama dhidi yake, na Baasha akamuua kule Gibethoni,^f jiji la Wafilisti, wakati Nadabu na Waisraeli wote walipokuwa wakilizingira Gibethoni.

28 Kwa hiyo Baasha akamuua katika mwaka wa tatu wa Mfalme Asa wa Yuda, akawa mfalme baada yake. **29** Mara tu alipokuwa mfalme, aliingamiza nyumba yote ya Yeroboamu. Hakumwacha mtu yeyote wa Yeroboamu akipumua; aliagiza waangamizwe kama Yehova alivyokuwa amesema kupitia Ahiya, mtumishi wake kutoka Shilo.^g **30** Alifanya hivyo kwa sababu ya dhambi ambazo Yeroboamu alikuwa ametenda na kusababisha Waisraeli wazitende na kwa sababu alikuwa amemkasirisha sana Yehova Mungu wa

15:23 *Au "aliyoimarisha; aliyojenga upya."

Israeli. **31** Na mambo mengi katika historia ya Nadabu, mambo yote aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **32** Na kulikuwa na vita daima kati ya Asa na Mfalme Baasha wa Israeli.^a

33 Katika mwaka wa tatu wa Mfalme Asa wa Yuda, Baasha mwana wa Ahiya akawa mfalme wa Waisraeli wote kule Tirsā, alitawala kwa miaka 24.^b **34** Lakini aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova,^c akafuata njia ya Yeroboamu na dhambi yake ambayo alisababisha Waisraeli kutenda.^d

16 Kisha neno hili la Yehova dhidi ya Baasha lika-mjia Yehu^e mwana wa Hanani:^f **2** “Nilikuinua kutoka mavumbini na kukufanya kuwa kiongozi wa watu wangu Waisraeli,^g lakini uliendelea kutembea katika njia ya Yeroboamu na kusababisha watu wangu Waisraeli watende dhambi hivi kwamba walinikasirisha kwa dhambi zao.^h **3** Kwa hiyo ninamfagilia mbali Baasha na nyumba yake, nami nitaifanya nyumba yake kuwa kama nyumba ya Yeroboamuⁱ mwana wa Nebati. **4** Mtu yeyote wa nyumba ya Baasha anayefia jijini ataliwa na mbwa; na mtu yeyote wa nyumba yake anayefia shambani ataliwa na ndege wa angani.”

5 Na mambo mengine katika historia ya Baasha, mambo aliyofanya na ukuu wake, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **6** Kisha Baasha akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake kule Tirsā; na Ela mwana wake akawa

SURA YA 15

a 2Nya 12:15

b 1Fa 16:8

c 1Fa 16:7

d 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33

SURA YA 16

e 2Nya 19:2
2Nya 20:34

f 2Nya 16:7

g 1Sa 2:8

h 1Fa 13:33

i 1Fa 14:10, 11
1Fa 15:29

j 1Fa 15:21, 33

Safu ya 2

a 1Fa 15:25-29

b 2Fa 9:31

c 1Fa 16:1-3

mfalme baada yake. **7** Tena, neno la Yehova dhidi ya Baasha na nyumba yake lilikuja kupitia nabii Yehu mwana wa Hanani, kwa sababu ya uovu wote aliotenda machoni pa Yehova na kumkasirisha kwa kazi za mikono yake, akawa kama nyumba ya Yeroboamu, na pia kwa sababu alimua Nadabu.^{*a}

8 Katika mwaka wa 26 wa Mfalme Asa wa Yuda, Ela mwana wa Baasha akawa mfalme wa Israeli kule Tirsā, naye alitawala kwa miaka miwili. **9** Zimri mtumishi wake, mkuu wa nusu ya kikosi chake cha magari ya vita, alipanga njama dhidi yake alipokuwa Tirsā akinywa na kulewa nyumbani kwa Arsa, msimamizi wa nyumba yake kule Tirsā. **10** Zimri akaingia, akampiga^b na kumuua katika mwaka wa 27 wa Mfalme Asa wa Yuda, naye akawa mfalme baada yake. **11** Alipokuwa mfalme, mara tu alipoketi kwenye kiti chake cha ufalme, aliangamiza nyumba yote ya Baasha. Hakumwacha wananamume yeyote,^{*} iwe ni mtu wake wa ukoo[†] au ni rafiki yake. **12** Basi Zimri akaiangamiza nyumba yote ya Baasha, kama Yehova alivyokuwa amesema dhidi ya Baasha kupitia nabii Yehu.^c **13** Alifanya hivyo kwa sababu ya dhambi zote ambazo Baasha na mwanawe Ela walikuwa wametenda na dhambi ambazo walisababisha Waisraeli kutenda na kumkasirisha Yeho-

16:7 *Yaani, mwana wa Yeroboamu. 16:11 *Tnn., “mtu yeyote anayekojoa ukutani.” Huu ni msemo wa Kiebrania wa kuwadarau wanaume. †Au “watu wanaolipiza kisasi chake cha damu.”

va Mungu wa Israeli kwa sanamu zao za ubatili.^a **14** Na mambo mengine katika historia ya Ela, mambo yote aliyofanya, je, haya jaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli?

15 Katika mwaka wa 27 wa Mfalme Asa wa Yuda, Zimri akawa mfalme kwa siku saba kule Tirsa wanajeshi walipokuwa wamepiga kambi dhidi ya Gibethoni,^b jiji la Wafilisti. **16** Baada ya muda wanajeshi waliokuwa wamepiga kambi wakasikia hivi: "Zimri amepanga njama na pia amemuua mfalme." Basi siku hiyo huko kambini Waisraeli wote wakamweka Omri,^c mkuu wa jeshi, kuwa mfalme wa Israeli. **17** Omri na Waisraeli wote wakapanda kutoka Gibethoni na kulizingira Tirsa. **18** Zimri alipoona kwamba jiji limetekwa, akaingia katika mnara wenye ngome wa nyumba ya mfalme* na kuiteketeza kwa moto akiwa ndani yake, naye akafa.^d **19** Alifanya hivyo kwa sababu ya dhambi zake mwenyewe alizofanya alipotenda maovu machoni pa Yehova kwa kuteembea katika njia ya Yeroboamu na kwa sababu ya dhambi aliyosababisha Waisraeli wafanye.^e **20** Na mambo mengine katika historia ya Zimri pamoja na njama yake, je, haya jaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli?

21 Wakati huo ndipo watu wa Israeli walipogawanyika makundi mawili. Kundi moja lilimfuata Tibni mwana wa Ginathi likitaka kumfanya kuwa

16:18 *Au "jumba la mfalme."

SURA YA 16

a Kum 32:21
1Sa 12:21
2Fa 17:15
Isa 41:29

b Yos 19:44, 48
Yos 21:20, 23
1Fa 15:27

c 2Fa 8:26
Mik 6:16

d Amu 9:53, 54
1Sa 31:4
2Sa 17:23

e 1Fa 12:28-30
1Fa 14:7,9

Safu ya 2

a 1Fa 20:1
2Fa 17:24
Amo 6:1
Mdo 8:5

b Mik 6:16

c 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33

d 1Fa 16:33
1Fa 21:4
1Fa 21:20-22
2Fa 10:1

mfalme, na kundi lingine likamfuata Omri. **22** Lakin watu waliokuwa wakimfuata Omri waliwashinda watu waliokuwa wakimfuata Tibni mwana wa Ginathi. Basi Tibni akafa, na Omri akawa mfalme.

23 Katika mwaka wa 31 wa Mfalme Asa wa Yuda, Omri akawa mfalme wa Israeli, naye akatawala kwa miaka 12. Alitawala Tirsa kwa miaka sita. **24** Alinunua mlima wa Samaria kutoka kwa Shemeri kwa talanta mbili za fedha,* akajenga jiji juu ya mlima huo. Jiji alilojenga aliliita Samaria,^{#a} jina la Shemeri mmiliki^a wa mlima huo. **25** Omri akaendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, akatenda maovu kuliko wote waliomtangulia.^b **26** Alitembea katika njia zote za Yeroboamu mwana wa Nebati na katika dhambi aliyokuwa amesababisha Waisraeli wafanye na kumkasirisha Yehova Mungu wa Israeli kwa sanamu zao za ubatili.^c **27** Na mambo mengine katika historia ya Omri, mambo aliyofanya na mambo makuu aliyotekeleza, je, haya jaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **28** Kisha Omri akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake huko Samaria; na Ahabu^d mwana wake akawa mfalme baada yake.

29 Ahabu mwana wa Omri akawa mfalme wa Israeli katika mwaka wa 38 wa Mfalme Asa wa Yuda, na Ahabu mwana wa Omri akatawala Israeli kwa miaka 22 huko

16:24 * Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. #Maana yake "Mali ya Ukoo wa Shemeri." ^aTnn., "bwana."

Samaria.^a **30** Ahabu mwana wa Omri alikuwa mwovu sana machoni pa Yehova kuliko wote waliomtangulia.^b **31** Na kana kwamba lilikuwa jambo dogo kwake kutembea katika dhambi za Yeroboamu^c mwana wa Nebati, hata alimwoa Yezebeli^d binti ya Ethbaali, mfalme wa Wasidoni,^e akaanza kumwabudu Baali^f na kumwinamia. **32** Isitoshe, alisimamisha madhabahu kwa ajili ya Baali katika nyumba ya Baali^g aliyojenga* kule Samaria. **33** Ahabu pia alitengeza mti mtakatifu.*^h Ahabu alifanya mambo mengi zaidi yaliyomkasirisha Yehova Mungu wa Israeli kuliko wafalme wote wa Israeli waliomtangulia.

34 Katika siku zake, Hieli kutoka Betheli alijenga upya Yeriko. Alipojenga mwingi wake, Abiramu mzaliwa wake wa kwanza alikufa, na alipoweka malango yake, Segubau mwana wake wa mwisho akafa, kama Yehova alivyokuwa amesema kupitia Yoshua mwana wa Nuni.ⁱ

17 Sasa Eliya*^j Mtishbi, mkaaji wa Gileadi,^k alimwambia hivi Ahabu: “Kwa hakika kama anavyoishi Yehova Mungu wa Israeli ninayemtumikia,[#] katika miaka hii hakutakuwa na umande wala mvua isipokuwa kwa neno langu!”^l

2 Neno hili la Yehova likamjia: **3** “Ondoka hapa, ugeuke kwenda upande wa mashariki, ujifiche katika Bonde*^m

16:32 *Au “hekalu la Baali alilojenga.”
16:33 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
17:1 *Maana yake “Mungu Wangu Ni Yehova.” #Tnn., “ninayesimama mbele zake.” 17:3, 5 *Au “Korongo.”

SURA YA 16

a 1Fa 16:23, 24
Isa 7:9

b 1Fa 16:25
1Fa 21:25
2Fa 3:1, 2

c 1Fa 12:28-30

d 1Fa 18:4, 19
1Fa 21:7
2Fa 9:30
Ufu 2:20

e Mwa 10:15

f Amu 2:11
Amu 10:6
2Fa 10:19
2Fa 17:16

g 2Fa 10:21, 27

h Kut 34:13
2Fa 10:26, 28
2Fa 13:6

i Yos 6:26

SURA YA 17

j 1Fa 17:15, 16
1Fa 17:22, 24
1Fa 18:36, 38
1Fa 18:46
2Fa 2:8, 11
Lu 1:17
Yoh 1:19, 21

k Yos 22:9

l Kum 28:15, 23
Yer 14:22
Lu 4:25
Yak 5:17

Safu ya 2

a Zb 37:25
Mt 6:11

b Hes 11:23
Amu 15:19

c 1Fa 18:5

d Lu 4:25, 26

e Ebr 11:32, 37

f 2Fa 4:2

la Kerithi, upande wa mashariki wa Yordani. **4** Utakunywa maji kutoka katika kijito, nami nitawaamuru kunguru wakuletee chakula huko.”^a **5** Akaenda mara moja na kutenda kulingana na neno la Yehova; alienda kukaa katika Bonde* la Kerithi, upande wa mashariki wa Yordani. **6** Na kunguru walikuwa wakimletea mkate na nyama asubuhi na mkate na nyama jioni, naye alikunywa maji kutoka katika kile kijito.^b **7** Lakin baada ya siku kadhaa, kijito hicho kikakauka^c kwa sababu mvua haikunyeshia nchini.

8 Basi neno hili la Yehova likamjia: **9** “Ondoka, nenda Sarefathi ya Sidoni, nawe ukae huko. Tazama! Nitamwamuru mjane fulani huko akupete chakula.”^d **10** Basi akainuka na kwenda Sarefathi. Alipofika kwenye lango la jiji, kulikuwa na mwanamke fulani mjane aliyekuwa akiokota kuni. Basi akamwita mwanamke huyo na kumwambia: “Tafadhali, niletee maji kidogo kwenye kikombe ninywe.”^e **11** Alipokuwa akienda kuyaleta, Eliya akamwita na kumwambia: “Tafadhali, niletee kipande cha mkate.” **12** Ndiipo mwanamke huyo akasema: “Kwa hakika kama Yehova Mungu wako anavyoishi, sina mkate, nina konzi moja tu ya unga katika mtungi mkubwa na mafuta kidogo katika mtungi mdogo.^f Sasa ninaokota kuni chache tu, kisha niende nyumbani na kupika chakula kidogo kwa ajili yangu na mwanangu. Baada ya kula chakula hicho, tutakufa.”

13 Kisha Eliya akamwambia: “Usiogope. Nenda nyu-

mbani ufanye kama ulivyo-sema. Lakini kwanza nitayarishie mkate mdogo wa mvingo kwa unga na mafuta uliyo nayo. Kisha unaweza kutayarisha chochote baadaye kwa ajili yako na mwanao. **14** Kwa maana Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: 'Unga ulio katika huo mtungi mkubwa hautakwisha, na mafuta yaliyo katika huo mtungi mdogo hayatakwisha mpaka siku ambayo Yehova ataleta mvua nchini.'" **15** Basi akaenda na kufanya kama Eliya alivyosema; mwanamke huyo pamoja na Eliya na familia ya mwanamke huyo wakawa na chakula kwa siku nyingi.^b **16** Unga uliokuwa katika mtungi huo mkubwa haukwisha, na mafuta yaliyokuwa katika mtungi ule mdogo hayakwisha, kama Yehova alivyokuwa amesema kupitia Eliya.

17 Baada ya mambo hayo, mwana wa mwanamke huyo mwenye nyumba akawa mgonjwa, na hali yake ikawa mba-ya sana hivi kwamba akakata pumzi.^c **18** Ndipo mwanamke huyo akamuuliza Eliya: "Nimekukosea nini, ewe mtu wa Mungu wa kweli? Je, ume-kuja kunikumbusha hatia yangu na kumuua mwanangu?"^d **19** Lakini Eliya akamwambia: "Nipe mwana wako." Kisha akamchukua kutoka mikono-ni mwake, akambeba hadi ka-tika chumba cha darini, ali-mokuwa akikaa, akamlaza kwenye kitanda chake mwe-nyewe.^e **20** Akamlilia Yehova kwa sauti akisema: "Ee Yehova Mungu wangu,^f je, unamdhuru pia mjane ninayekaa kwake kwa kumuua mwana-

SURA YA 17

a Zb 34:10
Zb 37:17,19
Flp 4:19

b Mt 10:41, 42
Lu 4:25, 26

c 2Fa 4:19, 20

d Ayu 13:26

e 2Fa 4:21, 32

f Zb 99:6

Safu ya 2

a Yak 5:16

b Kum 32:39
1Sa 2:6
2Fa 4:32, 34
2Fa 13:21
Lu 7:15
Lu 8:54, 55
Yoh 5:28, 29
Yoh 11:44
Mdo 9:40, 41
Mdo 20:9, 10
Ro 14:9
Ebr 11:17, 19

c Ebr 11:35

d Yoh 3:2

SURA YA 18

e Lu 4:25
Yak 5:17

f Zb 65:9, 10
Yer 14:22

g Law 26:26
Kum 28:24

h 1Fa 16:31

we?" **21** Kisha akajinyoosha juu ya mtoto huyo mara tatu na kumlilia Yehova kwa sauti akisema: "Ee Yehova Mungu wangu, tafadhali, acha uhai wa mtoto huyu umrudie." **22** Yehova akasikiliza ombi la Eliya,^a na uhai wa mtoto huyo ukamrudia, akawa hai tena.^b **23** Eliya akamchukua mtoto huyo, akamleta chini kutoka katika kile chumba cha darini, akampa mama yake; Eliya akasema: "Tazama, mwana wako yuko hai."^c **24** Ndipo mwanamke huyo akamwambia Eliya: "Sasa ninajua kwamba kwa kweli wewe ni mtu wa Mungu^d na kwamba neno la Yehova kutoka kinywani mwako ni kweli."

18 Baada ya muda fulani, katika mwaka wa tatu,^e neno la Yehova likamjia Eliya likisema: "Nenda ukamwone Ahabu, nami nitaleta mvua nchini."^f **2** Basi Eliya akaenda kumwona Ahabu, wakati huo kulikuwa na njaa kali sana^g Samaria.

3 Wakati huo, Ahabu akamwita Obadia, aliyekuwa msimamizi wa nyumba yake. (Obadia alimwogopa sana Yehova, **4** na Yezebeli^h alipokuwa akiwaua manabii wa Yehova, Obadia aliwachukua manabii 100 na kuwaficha katika mapango mawili, manabii 50 katika kila pango, naye alikuwa akiwapa mikate na maji.) **5** Kisha Ahabu akamwambia Obadia: "Pita kotekote nchini kwenye chemchemi zote za maji na mabonde* yote. Hue-nda tukapata majani ya kuto-sha ili farasi na nyumbu wae-ndeleo kuishi, wanyama wetu

18:5 *Au "makorongo."

wote wasife.” **6** Kwa hiyo wakagawana maeneo ya nchi ambako wangeenda kutafuta nyasi. Ahabu akaenda peke yake upande mmoja, na Obadia akaenda peke yake upande mwingine.

7 Obadia alipokuwa akienenda zake, akakutana na Eliya. Mara moja Obadia akamtambua, akaanguka chini kifudufudi na kumuuliza: “Je, ni wewe, bwana wangu Eliya?”^a **8** Akamjibu: “Ni mimi. Nenda ukamwambie bwana wako, ‘Eliya yuko hapa.’”

9 Lakini akasema: “Nimetenda dhambi gani hivi kwamba unanitia mimi mtumishi wako mikononi mwa Ahabu ili anieue? **10** Kwa hakika kama Yehova Mungu wako anavyoishi, hakuna taifa wala ufalme ambamo bwana wangu hakuwatuma watu wakutafute. Waliposema, ‘Hayuko hapa,’ aliagiza ufalme na taifa hilo liape kwamba limeshindwa kukupata.^b **11** Sasa unasema, ‘Nenda ukamwambie bwana wako: “Eliya yuko hapa.”’ **12** Nitakapokuacha, roho ya Yehova itakubeba na kukupeleka^c mahali ambapo sitajua, nami nikimwambia Ahabu naye asikupate, kwa hakika ataniau. Lakini mimi mtumishi wako nimemwogopa Yehova tangu nilipokuwa kijana. **13** Je, bwana wangu hukuambiwa niliyofanya Yezebeli alipokuwa akiwaua manabii wa Yehova, jinsi nilivyowaficha manabii 100 wa Yehova, manabii 50 katika kila pango, na jinsi nilivyokuwa nikiwapa mikate na maji?^d **14** Lakini sasa unasema, ‘Nenda ukamwambie bwana wako: “Eliya yuko hapa.”’ Hakika ataniau.”

SURA YA 18

a 2Fa 1:8

b 1Fa 17:2,3

c 2Fa 2:15,16
Mt 4:1
Mdo 8:39

d 1Fa 18:4

Safu ya 2

a Kut 20:4
1Fa 9:9
1Fa 16:30-33

b Yos 19:26,31

c 1Fa 16:33

d Yer 2:11
Ho 10:2
Mt 12:30
1Ko 10:21
2Ko 6:14,15e Kut 20:5
Yos 24:15
1Sa 7:3
Zb 100:3

f 1Fa 19:9,10

15 Hata hivyo, Eliya akamwambia: “Kwa hakika kama anavyoishi Yehova wa majeshi ninayemtumikia,* nitaenda kumwona leo.”

16 Basi Obadia akaenda kukutana na Ahabu na kumwambia habari hizo, kisha Ahabu akaenda kukutana na Eliya.

17 Mara tu Ahabu alipomwona Eliya akamwambia: “Kumbe ni wewe unayeiletea Israeli taabu kubwa!”*

18 Eliya akasema: “Sijailetea Israeli taabu, lakini ni wewe na nyumba ya baba yako mliofanya hivyo kwa kuziacha amri za Yehova na kufuata Mabaali.^a **19** Na sasa nikusanyie Waisraeli wote kwenye Mlima Karmeli,^b pamoja na manabii 450 wa Baali na manabii 400 wa mti mtaakatifu,^c wanaokula kwenye meza ya Yezebeli.” **20** Basi Ahabu akatuma ujumbe kwa Waisraeli wote, akawakusanya pamoja manabii kwenye Mlima Karmeli.

21 Kisha Eliya akawakaribia watu wote na kusema: “Mtaendelea kuyumbayumba kati ya maoni mawili tofauti*^d mpaka wakati gani? Ikiwa Yehova ndiye Mungu wa kweli, mfuateni;^e lakini ikiwa ni Baali, mfuateni!” Hata hivyo, watu hawakumjibu neno lolote. **22** Ndipo Eliya akawaambia watu: “Mimi peke yangu ndiye nabii wa Yehova aliyebaki,^f lakini manabii wa Baali ni 450. **23** Na watupatie ng’ombe dume wachanga wawili, kisha wachague ng’ombe

18:15 *Tnn., “ninayesimama mbele zake.” 18:17 *Au “unayesababisha Israeli itengwe.” 18:19 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 18:21 *Au “kuchechea kwa kutumia magongo mawili.”

dume mmoja mchanga na kumkata vipandevipande na kuviweka juu ya kuni, lakini wasiwashe moto. Nitamtayarisha ng'ombe dume mchanga wa pili na kumweka juu ya kuni, lakini sitawasha moto. **24** Kisha mtaliita jina la mungu wenu,^a nami nitaliita jina la Yehova. Mungu atakayejibu kwa moto, atathibitisha kwamba yote ndiye Mungu wa kweli.”^b Ndipo watu wote wakasema: “Jambo unalosema ni jema.”

25 Sasa Eliya akawaambia manabii wa Baali: “Chagueni ng'ombe dume mmoja mchanga na kumtayarisha kwanza, kwa sababu ninyi ni wengi. Kisha mliite jina la mungu wenu, lakini msiwashe moto.” **26** Basi waka-mchukua huyo ng'ombe dume mchanga waliyepewa, waka-mtayarisha, na kuendelea kuliita jina la Baali kuanzia asubuhi mpaka aduhuri, wakisema: “Ee Baali, tujibu!” Lakini hapakuwa na sauti yoyote, wala yeyote aliyewajibu.^c Nao wakazidi kurukaruka kuizunguka madhabahu waliyokuwa wametengeneza. **27** Karibu wakati wa aduhuri Eliya akaanza kuwadhihaki na kusema: “Iteni kwa sauti yenu yote! Je, si yeye ni mungu?”^d Labda amezama katika mawazo au ameenda chooni.* Au pengine amelala usingizi na mtu fulani anahitaji kumwamsha!” **28** Walikuwa wakiita kwa sauti yao yote na kujikatakata kwa visu na mikuki, kulingana na desturi yao, mpaka walipotokwa na damu nyingi mwili mzima. **29** Wakati wa adhu-

SURA YA 18

a Amu 6:31

b Law 9:23, 24
Kum 4:24
Amu 6:21
1Nya 21:26
2Nya 7:1c Isa 45:20
Yer 10:5
Da 5:23
Hab 2:18, 19
1Ko 8:4

d Isa 41:23

Safu ya 2

a Isa 44:19, 20

b 1Fa 19:14

c Mwa 32:28, 30
Mwa 35:10
Isa 48:1d Kut 20:25
Kum 27:6e Mwa 22:9
Law 1:7, 8

f Kut 29:41

g Mwa 26:24

h Mwa 28:13

huri ukapita lakini wakaendelea kutenda kiwazimu* mpaka jioni wakati ambapo toleo la nafaka hutolewa, lakini hapakuwa na sauti yoyote wala yeyote aliyejibu; hakuna aliye-wasikiliza.^a

30 Hatimaye Eliya akawaambia watu wote: “Nikaribieni.” Basi watu wote wakamkaribia. Kisha akairekebisha madhabahu ya Yehova iliyokuwa imebomolewa.^b **31** Halafu Eliya akachukua mawe 12, kulingana na idadi ya makabila ya wana wa Yakobo, ambaye neno la Yehova lilikuwa limemjia likisema: “Jina lako litakuwa Israeli.”^c **32** Akatumia mawe hayo kujenga madhabahu^d katika jina la Yehova. Kisha akachimba mtaro kuzunguka madhabahu hiyo, eneo kubwa ambalo lilitosha kupandwa sea mbili* za mbegu. **33** Kisha akapanga kuni, akamkata yule ng'ombe dume mchanga vipandevipande na kuviweka juu ya hizo kuni.^e Halafu akasema: “Ijaze-ni maji mitungi mikubwa minne, myamwage juu ya dhahibi ya kuteketezwa na juu ya kuni.” **34** Kisha akasema: “Fanyeni hivyo tena.” Basi wakafanya hivyo tena. Akasema tena: “Fanyeni hivyo mara ya tatu.” Basi wakafanya hivyo mara ya tatu. **35** Maji yaka-jaa kuizunguka madhabahu, na pia akaujaza mtaro maji.

36 Karibu wakati wa kutoa toleo la nafaka la jioni,^f nabii Eliya akaja mbele na kusema: “Ee Yehova, Mungu wa Abrahamu,^g Isaka,^h na Israeli, acha leo ijulikane kwamba

18:29 *Au “kama manabii.” 18:32 *Sea moja ilikuwa sawa na lita 7.33 (vibaba 6.66). Angalia Nyongeza B14.

18:27 *Au labda, “amesafiri.”

wewe ni Mungu katika Israeli na kwamba mimi ni mtumishi wako na kwamba nimefanya mambo haya yote kwa neno lako.^a **37** Nijibu, Ee Yehova! Nijibu ili watu hawa wajue kwamba wewe, Yehova, ndiye Mungu wa kweli na kwamba wewe unaigeuza mioyo yao ikurudie.”^b

38 Ndipo moto wa Yehova ukashuka kutoka juu, ukaitetekeza hiyo dhabihu ya kuteketezwa,^c kuni, mawe, na mavumbi, nao ukayaramba maji yaliyokuwa mtaroni.^d **39** Watu wote walipoona jambo hilo, mara moja wakaaunguka chini kifudufudi na kusema: “Yehova ndiye Mungu wa kweli! Yehova ndiye Mungu wa kweli!” **40** Kisha Eliya akawaambia: “Wakamate ni manabii wa Baali! Msimwache hata mmoja wao atoroke!” Mara moja wakawakamata, na Eliya akawaleta chini kwenye kijito cha* Kishoni^e na kuwachinja huko.^f

41 Sasa Eliya akamwambia Ahabu: “Panda juu, ukale na kunywa, kwa maana kuna sauti ya mvua kubwa sana.”^g **42** Basi Ahabu akapanda juu kwenda kula na kunywa, lakini Eliya akapanda kwenye kilele cha Karmeli, akajikunyata ardhini, uso wake ukiwa katikati ya magoti yake.^h **43** Kisha akamwambia mtumishi wake: “Panda juu, tafadhali, utazame upande wa bahari.” Basi akapanda juu, akatazama na kusema: “Hakuna kitu chochote.” Eliya akamwambia mara saba, “Rudi.” **44** Mara ya saba mtumishi wake akamwa-

18:40 *Au “korongo la.”

SURA YA 18

a Hes 16:28
Yoh 11:42

b Yer 31:18
Eze 33:11

c Law 9:23, 24
Amu 6:21
2Nya 7:1

d 1Fa 18:23, 24

e Amu 5:20, 21
Zb 83:9

f Kum 13:1-5
Kum 18:20

g 1Fa 17:1

h Yak 5:17, 18

Safu ya 2

a 1Sa 12:18
Ayu 38:37

b Yos 19:17, 18
1Fa 21:1

SURA YA 19

c 1Fa 16:29
1Fa 21:25

d 1Fa 16:31

e 1Fa 18:40

f Kut 2:15
1Sa 27:1

g Mwa 21:31

h Yos 15:21, 28

i Hes 11:15
Ayu 3:21
Yon 4:3

j Da 10:8-10
Mdo 12:7

k Zb 34:7
Ebr 1:7, 14

mbia: “Tazama! Kuna wingu dogo kama mkono wa mwana-damu linalopanda kutoka baharini.” Ndipo Eliya akasema: “Nenda, mwambie hivi Ahabu: ‘Funga farasi kwenye gari! Teremka ili mvua kubwa isiku-zuie!’” **45** Wakati huo, mawingu mazito yakatanda angani, upepo ukavuma, na mvua kubwa sana ikanyesha;^a naye Ahabu akaendesha gari mpa-ka Yezreeli.^b **46** Lakini mkono wa Yehova ukaja juu ya Eliya, akajifunga vazi lake kiunoni, akakimbia na kumpita Ahabu na kutangulia kufika Yezreeli.

19 Kisha Ahabu^c akamwambia Yezebeli^d mambo yote ambayo Eliya alikuwa amefanya na jinsi alivyowaua manabii wote kwa upanga.^e **2** Ndipo Yezebeli akamtuma mjumbe kwa Eliya, aki-sema: “Miungu na iniadhibu, tena vikali, ikiwa kufikia kesho wakati kama huu sitakufanya uwe kama* kila mmoja wa manabii hao!” **3** Basi Eliya akaogopa, akaondoka na kukimbia ili kuokoa uhai wake.^{*f} Akafika Beer-sheba,^g jiji la Yuda,^h akamwacha mtumishi wake huko. **4** Akaingia nyikani safari ya siku moja, akafika na kuketi chini ya mti wa mretemu, naye akaomba afe. Akasema: “Imetosha! Sasa, Ee Yehova, niue,^{*i} kwa sababu mimi si bora kuliko mababu zangu.”

5 Kisha akalala chini na kushikwa na usingizi chini ya mti huo wa mretemu. Lakini kwa ghafla malaika akamgusa/na kumwambia: “Amka, ule.”^k

19:2 *Au “sitafanya nafsi yako iwe kama nafsi ya.” 19:3 *Au “nafsi yake.” 19:4 *Au “iondoa nafsi yangu.”

6 Alipoangalia, aliona karibu na kichwa chake mkate wa mvingo ukiwa juu ya mawe yenye moto na pia gudulia la maji. Akala na kunywa na kulala chini tena. 7 Baadaye malaika wa Yehova akarudi mara ya pili, akamgusa na kusema: “Amka, ule, kwa maana safari itakuwa ngumu sana kwako.” 8 Basi akaamka, akala na kunywa, na kwa nguvu za chakula hicho akasafiri kwa siku 40, mchana na usiku, mpaka alipofika Horebu, mlima wa Mungu wa kweli.^a

9 Huko akaingia pangoni^b na kulala humo usiku; na tazama! neno la Yehova likamjia na kumuuliza: “Unafanya nini hapa, Eliya?” 10 Akajibu: “Nimekuwa na bidii kwelikweli kwa ajili ya Yehova Mungu wa majeshi;^c kwa maana Waisraeli wameliacha agano lako,^d wamebomoa madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga,^e nimebaki mimi peke yangu. Sasa wanataka kuniua.”^{*f} 11 Lakini Akasema: “Toka nje, ukasimani mlimani mbele za Yehova.” Na tazama! Yehova alikuwa akipita karibu,^g na upepo mkali na wenye nguvu ulikuwa ukipasua milima na kuvunja miamba mbele za Yehova,^h lakini Yehova hakuwa katika upepo huo. Baada ya upepo, kukawa na tetemeko la ardhi,ⁱ lakini Yehova hakuwa katika tetemeko hilo. 12 Baada ya tetemeko la ardhi, kukawa na moto,^j lakini Yehova hakuwa katika moto huo. Baada ya moto, kukawa na sauti tulivu, ya chini.^k 13 Mara tu Eliya alipoisi-

19:10, 14 *Au “kuiondoa nafsi yangu.”

SURA YA 19

- a Kut 3:1
Kut 19:18
Mal 4:4
- b Ebr 11:32, 38
- c Kut 20:4, 5
Hes 25:11
Zb 69:9
- d Kum 29:24, 25
Amu 2:20
1Fa 8:9
2Fa 17:15
- e 1Fa 18:4
- f 1Fa 19:2
Ro 11:2, 3
- g Kut 33:22
- h Zb 50:3
Isa 29:6
- i 1Sa 14:15
Ayu 9:6
Zb 68:8
Nah 1:5
- j Kum 4:11
- k Kut 34:5, 6

Safu ya 2

- a Kut 3:6
- b Kum 31:20
Zb 78:37
Isa 1:4
Yer 22:9
- c Ro 11:2, 3
- d 2Fa 8:7, 8
Amo 1:4
- e 2Fa 9:1-3
2Fa 9:30-33
- f 2Fa 2:9, 15
- g 2Fa 8:12
2Fa 10:32
2Fa 13:3
- h 2Fa 9:14, 24
2Fa 10:6, 7
2Fa 10:23, 25
- i 2Fa 2:23, 24
- j Ro 11:4
- k Kut 20:5
- l Ho 13:2
- m 2Fa 2:8

kia, aliufunika uso wake kwa vazi lake rasmi,^a akatoka nje na kusimama kwenye mlango wa pango. Kisha sauti ikamuuliza: “Unafanya nini hapa, Eliya?” 14 Akasema: “Nimekuwa na bidii kwelikweli kwa ajili ya Yehova Mungu wa majeshi; kwa maana Waisraeli wameliacha agano lako,^b wamebomoa madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga, nimebaki mimi peke yangu. Sasa wanataka kuniua.”^{*c}

15 Yehova akamwambia: “Rudi, nenda katika nyika ya Damasko. Utakapofika huko, mtie mafuta Hazaeli^d awe mfalme wa Siria. 16 Pia unapaswa kumtia mafuta Yehu^e mjukuu wa Nimshi awe mfalme wa Israeli, na umtie mafuta Elisha mwana wa Shafati kutoka Abel-mehola awe nabii baada yako.^f 17 Mtu yeyote atakayeponyoka upanga wa Hazaeli,^g Yehu atamuua;^h na yeyote atakayeponyoka upanga wa Yehu, Elisha atamuua.ⁱ 18 Na bado nina watu 7,000 waliobaki Israeli,^j watu wote ambao hawakumpigia magoti Baali,^k na ambao hawakumbusu kwa midomo yao.”^l

19 Basi akaondoka huko, akamkuta Elisha mwana wa Shafati akilima kwa jozi 12 za ng'ombe dume, naye alikuwa na jozi ya 12. Basi Eliya akamkaribia, akalitupa vazi lake rasmi^m juu yake. 20 Ndipo akawaacha wale ng'ombe dume, akamfuata Eliya mbio na kusema: “Tafadhali, niruhusu nimbusu baba yangu na mama yangu. Kisha nitakufuata.” Eliya akamwambia: “Nenda, rudi nyumbani, nimekuzaia kwa njia gani?” 21 Basi akarudi, akachukua jozi moja

ya ng'ombe dume na kuwatoa dhabihu, naye akatumia vifaa vya kulimia kuchemsha nyama ya ng'ombe dume hao, kisha akawapa watu, nao wakala. Baada ya hapo akaondoka na kumfuata Eliya na kuanza kumhudumia.^a

20 Basi Mfalme Benhadadi^b wa Siria^c akakusanya jeshi lake lote pamoja na wafalme wengine 32 wakiwa na farasi wao na magari yao ya vita; akapanda kwenda kuzingira^d jiji la Samaria^e na kupigana nalo. **2** Kisha akawatuma wajumbe kwa Mfalme Ahabu^f wa Israeli jijini, akamwambia: "Benhadadi anasema, **3** 'Fedha yako na dhahabu yako ni yangu, na pia wake zako warembo zaidi na wana wako ni wangu.'" **4** Ndipo mfalme wa Israeli akasema: "Kama ulivyosema bwana wangu mfalme, mimi ni wako pamoja na vitu vyangu vyote."^g

5 Baadaye wajumbe hao wakarudi na kusema: "Benhadadi anasema, 'Nilituma ujumbe huu kwako: "Utani-pa fedha yako, dhahabu yako, wake zako, na wana wako.'" **6** Lakini kesho wakati kama huu nitawatuma watumishi wangu kwako, nao wataichunguza kwa makini nyumba yako na nyumba za watumishi wako, watachukua vitu vyako vyote vinavyotamanika na kwenda navyo."

7 Ndipo mfalme wa Israeli akawaita wazee wote wa nchi na kuwaambia: "Angalieni, tafadhali, na mjue kwamba mtu huyu anakusudia kuleta msiba, kwa maana alitaka nimpe wake zangu, wanangu, fedha yangu, na dhahabu yangu, nami sikukataa agizo lake."

SURA YA 19

a Kut 24:13
2Fa 2:3
2Fa 3:11

SURA YA 20

b 2Fa 8:7

c 2Sa 8:6
2Fa 5:2
Isa 9:12

d Kum 28:52

e 2Fa 6:24
2Fa 17:5

f 1Fa 16:29

g Kum 28:15, 48

Safu ya 2

a Met 16:18
Met 27:1
Mhu 7:8

b 1Fa 16:29

c Kut 14:18
Zb 37:20

8 Ndipo wazee wote na watu wote wakamwambia: "Usitii, wala kukubali." **9** Kwa hiyo akawaambia wajumbe wa Benhadadi: "Mwambieni bwana wangu mfalme, 'Mambo yote ambayo ulitaka mwanzoni mimi mtumishi wako nifanye nitafanya, lakini siwezi kufanya jambo hili.'" Basi wajumbe hao wakaenda zao, wakampelekea ujumbe hao.

10 Kisha Benhadadi akatuma ujumbe huu kwake: "Miu-ngu na iniadhibu, tena vikali, ikiwa kuna mavumbi ya kutosha Samaria hivi kwamba kila mtu anayenifuata anaweza kupata konzi moja!"

11 Mfalme wa Israeli akajibu hivi: "Mwambieni, 'Anayevaa silaha zake hapaswi kujigamba kama mtu anayezivua.'"^a

12 Mara tu Benhadadi aliposikia jibu hilo, yeye na wale wafalme walipokuwa wakinywa katika mahema yao,^{*} akawaambia watumishi wake: "Jitayarisheni kushambulia!" Basi wakajitayarisha kushambulia jiji hilo.

13 Lakini nabii fulani akaenda kwa Mfalme Ahabu^b wa Israeli na kumwambia: "Yehova anasema, 'Je, umeuona umati huu wote mku-bwa? Tazama, ninautia mikononi mwako leo, kisha utajua kwamba mimi ni Yehova.'"^c

14 Ahabu akauliza: "Kupitia nani?" Nabii huyo akasema: "Yehova anasema hivi: 'Kupitia watumishi wa wakuu wa mikoa.'"^{*} Ndipo Ahabu akamuuliza: "Ni nani atakayeanzisha vita?" Nabii huyo akasema: "Ni wewe!"

20:12 * Au "vibanda vyao." 20:14 * Au "wilaya za utawala."

15 Kisha Ahabu akawahe-sabu watumishi wa wakuu wa mikoa, nao walikuwa 232; halafu akawahesabu wanau-me wote wa Israeli, walikuwa 7,000. 16 Wakaondoka wakati wa adhuhuri Ben-hadadi alipokuwa akinywa na kulewa katika mahema* pamoja na wale wafalme 32 waliokuwa wakimsaidia. 17 Watumishi wa wakuu wa mikoa walipotoka kwanza, mara moja Ben-hadadi akawatuma wajumbe. Wakamletea habari hii: "Wanaume wamekuja kutoka Samaria." 18 Ndipo akasema: "Ikiwa wamekuja kwa amani, waleteni wakiwa hai; ikiwa wamekuja kwa ajili ya vita, bado mnapaswa kuwaleta wakiwa hai." 19 Lakini watu hao walipotoka jijini—watumishi wa wakuu wa mikoa na majeshi yaliyokuwa yakiwafuata— 20 kila mmoja wao akamuua adui yake. Ndipo Wasiria wakakimbia,^a na Waisraeli wakawafuatia, lakini Mfalme Ben-hadadi wa Siria akapanda farasi na kutoroka pamoja na baadhi ya wapanda farasi. 21 Lakini mfalme wa Israeli akatoka na kuendelea kuwaua maadui waliopanda farasi na magari, naye akapata ushindi mkubwa dhidi ya Wasiria.*

22 Baadaye nabii huyo^b akaenda kwa mfalme wa Israeli na kumwambia: "Nenda, jii-marishe na ufikirie jambo utakalofanya,^c kwa maana mwanzoni mwa mwaka ujao* mfalme wa Siria atakuja kuku-shambulia."^d

23 Sasa watumishi wa mfalme wa Siria wakamwambia:

20:16 *Au "vibanda." 20:21 *Au "akawachinja Wasiria wengi." 20:22 *Yaani, majira yajayo ya kuchipua.

SURA YA 20

a Law 26:8
Kum 28:7

b 1Fa 20:13

c Met 20:18

d 2Sa 11:1

Safu ya 2
a 1Fa 20:1,16

b 2Fa 13:17

c Amu 6:5, 6
1Sa 13:5
2Nya 32:7

d Kum 32:26, 27
Eze 20:9
Eze 36:22

e Kut 6:7
Kut 7:5
Zb 83:18
Eze 6:14
Eze 39:7

"Mungu wao ni Mungu wa milima. Ndiyo sababu walitushinda nguvu. Lakini tukipigana nao kwenye nchi tambarare, tutawashinda nguvu. 24 Fanya hivi pia: Waondoe wafalme wote^a katika nafasi zao, na mahali pao uweke magavana. 25 Kisha ukusanye* jeshi linalolingana na jeshi ulilopoteza, farasi kwa farasi na gari kwa gari. Acha tupigane nao kwenye nchi tambarare, na hakika tutawashinda nguvu." Basi akasikiliza ushauri wao na kufanya kama walivyosema.

26 Mwanzoni mwa mwaka,* Ben-hadadi akawakusanya Wasiria, akapanda kwenda Afe-ki^b ili kupigana na Waisraeli. 27 Waisraeli pia walikusanywa kwa ajili ya vita na kupewa vitu walivyohitaji, nao wakatoka kwenda kukabiliana nao. Waisraeli walipopiga kambi mbele yao, walikuwa kama vikundi viwili vidogo vya mbuzi, lakini Wasiria walijaa kote nchini.^c 28 Kisha yule mtu wa Mungu wa kweli akaenda kwa mfalme wa Israeli na kumwambia: "Yehova anasema hivi, 'Kwa sababu Wasiria wamesema: "Yehova ni Mungu wa milima, wala si Mungu wa nchi tambarare," nitautia umati huu wote mkubwa mkononi mwako,^d na hakika utajua kwamba mimi ni Yehova."^e

29 Wakaendelea kupiga kambi wakielekeana kwa siku saba, na katika siku ya saba vita vikaanza. Kwa siku moja, Waisraeli wakawaua wanajeshi 100,000 Wasiria wanaotembea kwa miguu. 30 Wanajeshi waliobaki wakakimbilia

20:25 *Tnn., "hesabu." 20:26 *Yaani, majira ya kuchipua.

Afeki,^a ndani ya jiji. Lakini ukuta ukawaangukia wanau-me 27,000 kati ya wale walio-kuwa wamebaki. Ben-hadadi pia akakimbia na kuingia jijini, akajificha katika chumba fulani cha ndani.

31 Kwa hiyo watumishi wake wakamwambia: "Tazama, tumesikia kwamba wafalme wa nyumba ya Israeli ni wafalme wenye rehema.* Tafadhali, turuhusu tuvae nguo za magunia viunoni na kufunga kamba vichwani kisha twende kwa mfalme wa Israeli. Huenda akakuacha hai."^{#b}

32 Basi wakavaa nguo za magunia viunoni na kufunga kamba vichwani, wakaenda kwa mfalme wa Israeli na kumwambia: "Mtumishi wako Ben-hadadi anasema, 'Tafadhali, niruhusu niishi.'"^{*} Akasema: "Je, angali hai? Yeye ni ndugu yangu." **33** Basi watu hao wakaliona jambo hilo kuwa ishara njema, na bila kukawia wakaamini maneno yake, wakamwambia: "Ben-hadadi ni ndugu yako." Kwa hiyo akasema: "Nendeni mkamlete." Kisha Ben-hadadi akatoka na kwen-nda kwake, mfalme akampandisha garini.

34 Sasa Ben-hadadi akamwambia: "Majiji ambayo baba yangu alichukua kutoka kwa baba yako nitayarudisha, nawe unaweza kujianzishia masoko* Damasko, kama baba yangu alivyofanya Samaria."

Ahabu akamwambia, "Kwa msingi wa makubaliano haya,[#] nitakuruhusu uende."

20:31 *Au "upendo mshikamanifu."

[#]Au "huenda akaiacha hai nafsi yako."

20:32 *Au "iruhusu nafsi yangu iishi."

20:34 *Au "kujichagulia mitaa."

[#]Au "agano hili."

SURA YA 20

a 1Fa 20:26

b Yon 3:8, 9

Safu ya 2

a 2Fa 2:3

b 2Fa 10:24

Mdo 12:19

Mdo 16:27

Basi akafanya makubaliano naye na kumruhusu aende zake.

35 Kwa neno la Yehova, mmoja wa wana wa manabii^{*a} akamwambia mwenzake: "Tafadhali, nipige." Lakini mtu huyo akakataa kumpiga.

36 Basi akamwambia: "Kwa sababu hukuisikiliza sauti ya Yehova, mara tu tutakapochana, simba atakuua." Wali-poachana, simba akatokea na kumuua.

37 Akamkuta mtu mwingine na kumwambia: "Tafadhali, nipige." Mtu huyo akampiga na kumjeruhi.

38 Kisha nabii huyo akaenda na kumsubiri mfalme kando ya barabara, akafunika macho yake kwa kitambaa ili aufiche uso wake. **39** Mfalme alipokuwa akipita, akamlilia mfalme akisema: "Mimi mtumishi wako nilienda sehemu ambayo mapambano yalikuwa makali vitani, na mtu fulani alikuwa akitoka vitani akaniletea mwanamume mmoja na kuniambia, 'Mlinde mtu huyu. Akitoroka, utalipia uhai wake kwa uhai wako,^{*b} la si-vyo utalipa talanta moja[#] ya fedha.' **40** Na mimi mtumishi wako nilipokuwa nikishughulika hapa na pale, kwa ghafila mtu huyo akatoroka." Mfalme wa Israeli akamwambia: "Hivyo ndivyo utakavyohukumiwa; umejihukumu mwenyewe." **41** Kisha akaonda haraka kitambaa kilichofunika macho yake, na mfalme

20:35 *Inaonekana maneno "wana wa manabii" yanarejelea shule ya kuwafundisha manabii au chama cha manabii.

20:39 *Au "nafsi yake kwa nafsi yako."

[#]Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

wa Israeli akatambua kwamba alikuwa mmoja wa manabii.^a **42** Mtu huyo akamwambia mfalme: “Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu ume-mwacha atoroke kutoka mikononi mwako mtu ambaye nilisema anapaswa kuuawa,^b utalipia uhai wake kwa uhai wako,^{*c} na watu wako watachukua mahali pa watu wake.”^d **43** Ndipo mfalme wa Israeli akaenda nyumbani Samaria,^e akiwa amesononeka na kuvunjika moyo.

21 Baada ya hayo, jambo fulani lilitendeka kuhusiana na shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli; lilikuwa Yezreeli,^f kando ya jumba la Mfalme Ahabu, mfalme wa Samaria. **2** Ahabu akamwambia Nabothi: “Nipe shamba lako la mizabibu ili nilifanye kuwa shamba la mboga, kwa sababu liko karibu na nyumba yangu. Badala ya shamba hilo, nitakupa shamba bora zaidi la mizabibu. Au ukipenda, nitakulipa pesa zinazolingana na thamani yake.” **3** Lakini Nabothi akamwambia Ahabu: “Ni jambo nisiloweza kamwe kuwazia, kulingana na maoni ya Yehova, kukupa urithi wa mababu zangu.”^g **4** Basi Ahabu akaingia nyumbani mwake, akiwa amesononeka na kuvunjika moyo kwa sababu ya jibu ambalo Nabothi Myezreeli alimpa aliposema: “Sitakupa urithi wa mababu zangu.” Kisha akalala kitandani mwake, akaugeuzia mbali uso wake, na kukataa kula.

5 Yezebeli mke wake^h akaingia ndani kumwona, akamu-

20:42 *Au “nafsi yake kwa nafsi yako.”

SURA YA 20

a 1Fa 20:35

b Law 27:29
1Sa 15:9
Yer 48:10c 1Fa 22:31, 35
2Nya 18:33d 2Fa 6:24
2Fa 8:12
2Nya 18:16

e 1Fa 16:29

SURA YA 21

f Yos 19:17, 18

g Law 25:23
Hes 36:7h 1Fa 16:31
1Fa 18:4
1Fa 19:2
1Fa 21:25

Safu ya 2

a Mik 2:1
Mik 7:3b Ne 9:38
Est 8:8

c Kum 16:18

d Kut 20:16
Kum 17:6

e Kut 22:28

f Law 24:16
Yoh 10:33

liza, “Kwa nini umehuzunika* sana hivi kwamba unakataa kula?” **6** Akamjibu: “Ni kwa sababu nilimwambia Nabothi Myezreeli, ‘Niuzie shamba lako la mizabibu. Au ukipenda, nitakupa shamba lingine la mizabibu badala ya shamba hilo.’ Lakini akaniambia, ‘Sitakupa shamba langu la mizabibu.’” **7** Yezebeli mke wake akamwambia: “Je, si wewe unayetawala ukiwa mfalme wa Israeli? Inuka, kula chakula, moyo wako na uchanga-mke. Nitakupa shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli.”^a **8** Basi Yezebeli akaandika barua kwa jina la Ahabu, akazipiga muhuri wa Ahabu^b na kuzituma barua hizo kwa wazee^c na wakuu walioishi katika jiji la Nabothi. **9** Aliandika hivi katika barua hizo: “Tangazeni watu wafunge, halafu mketisheni Nabothi mbele ya watu. **10** Nanyi muwaketishe watu wawili wasiofaa kitu mbele yake ili watoe ushahidi dhidi yake,^d wakisema, ‘Umemtukana Mungu na mfalme!’^e Kisha mtoeni nje na kumuua kwa kumpiga mawe.”^f

11 Basi watu wa jiji lake, wazee na wakuu walioishi katika jiji lake, wakafanya kama ilivyoandikwa katika barua ambazo Yezebeli aliwatumia. **12** Wakatangaza watu wafunge, kisha wakamketisha Nabothi mbele ya watu. **13** Ndipo watu wawili miongoni mwa watu wasiofaa kitu wakaja na kuketi mbele yake, nao wakaanza kutoa ushahidi dhidi ya Nabothi mbele ya watu, wakisema: “Nabothi amemtukana Mungu na

21:5 *Tnn., “Kwa nini roho yako imehuzunika.”

mfalme!"^a Kisha wakamtoa nje ya jiji, wakamuua kwa kumpiga mawe.^b **14** Halafu wakamtumia Yezebeli ujumbe huu: "Nabothi ameua kwa kupigwa mawe."^c

15 Mara tu Yezebeli aliposikia kwamba Nabothi amepigwa mawe akafa, akamwambia Ahabu: "Inuka, chukua shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli,^d ambalo alikataa kukuuzia, kwa maana Nabothi hayuko hai tena. Amekufa." **16** Mara tu Ahabu aliposikia kwamba Nabothi amekufa, Ahabu aliondoka, akashuka kwenda kwenye shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli ili alichukue.

17 Lakini neno la Yehova likamjia Eliya^e Mtishbi, likisema: **18** "Ondoka, nenda ukutane na Ahabu mfalme wa Israeli huko Samaria.^f Yuko katika shamba la mizabibu la Nabothi, ameenda huko kulichukua. **19** Mwambie hivi: 'Yehova anauliza hivi: "Je, umemua mtu^g na kuchukua mali yake?"'^h Kisha mwambie, 'Yehova anasema hivi: "Mahali ambapo mbwa waliramba damu ya Nabothi, ndipo watakapoiramba damu yako mweenyewe."ⁱ

20 Ahabu akamwambia Eliya: "Yaani unenipata, ewe adui yangu?"^j Akajibu: "Nimekupata. 'Kwa sababu umeazimia* kutenda maovu machoni pa Yehova,^k **21** sasa ninakuletea msiba, nami nitafagia kabisa baada yako na kumwangamiza kila mwanamume*"

21:20 *Tnn., "umejiuza." 21:21 *Tnn., "mtu yeyote anayekojoa ukutani." Huu ni msemu wa Kiebrania wa kuwadharau wanaume.

SURA YA 21

a Amo 5:12
Hab 1:4

b 2Fa 9:25, 26
Mhu 4:1

c Mhu 5:8
Mhu 8:14
Hab 1:13

d 1Fa 21:7

e 1Fa 17:1

f 1Fa 16:29

g Mwa 4:8, 10

h Kum 5:21
Hab 2:9

i 1Fa 22:37, 38
2Fa 9:25, 26

j 1Fa 18:17
Amo 5:10

k 1Fa 16:30

Safu ya 2

a 2Fa 10:7, 17

b 2Fa 9:7-9

c 1Fa 15:25-29

d 1Fa 16:3, 11

e 2Fa 9:10, 35

f 1Fa 14:11
1Fa 16:4

g 1Fa 16:30

h 1Fa 16:31
2Nya 22:2, 3
Ufu 2:20

i Kut 23:28
Kum 9:5

j Zb 78:34

k 2Fa 9:25, 26
2Fa 10:7, 11

wa Ahabu,^a kutia ndani wasio na uwezo na walio dhaifu katika Israeli.^b **22** Nami nitafanya nyumba yako iwe kama nyumba ya Yeroboamu^c mwana wa Nebati na kama nyumba ya Baasha^d mwana wa Ahiya, kwa sababu umenikasirisha na kusababisha Waisraeli wataende dhambi.' **23** Pia Yehova anasema hivi kumhusu Yezebeli: 'Mbwa watamla Yezebeli katika shamba la Yezreeli.^e **24** Mtu yeyote wa Ahabu anayefia jijini mbwa watamla, na yeyote anayefia shambani ndege wa angani watamla.^f **25** Kwa kweli, hajawahi kamwe kutokea mtu yeyote kama Ahabu,^g aliyeeazimia kabisa* kutenda maovu machoni pa Yehova, akichochewa na Yezebeli mke wake.^h **26** Alitenda kwa njia yenye kuchukiza kabisa kwa kufuata sanamu zenye kuchukiza,* kama Waamori wote walivyo kuwa wamefanya, ambao Yehova aliwafukuza kutoka mbele ya Waisraeli.'ⁱ

27 Mara tu Ahabu aliposikia maneno hayo, akararua mavazi yake na kuvaa nguo za magunia; akaanza kufunga na kulala chini katika nguo za magunia na kutembea kwa huzuni. **28** Kisha neno hili la Yehova likamjia Eliya Mtishbi: **29** "Je, umeona jinsi ambavyo Ahabu amejinyenyekeza kwa sababu yangu?^j Kwa sababu amejinyenyekeza mbele zangu, sitauleta msiba huo akiwa hai. Nitaitetea nyumba yake msiba huo katika siku za mwanawe."^k

21:25 *Tnn., "aliyejiuza." 21:26 *Hue-nda neno la Kiebrania linahusiana na neno "mavi," nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

22 Kwa miaka mitatu haku-kuwa na vita kati ya Siria na Israeli. **2** Katika mwaka wa tatu, Mfalme Yehoshafati^a wa Yuda akashuka kwen-
da kwa mfalme wa Israeli.^b **3** Kisha mfalme wa Israeli akawaambia watumishi wake: “Je, mnajua kwamba Ramothi-gileadi^c ni jiji letu? Na bado tunasitasita kulichukua kutoka kwa mfalme wa Siria.” **4** Halafu akamuuliza Yehoshafati: “Je, utaenda pamoja nami kupigana kule Ramothi-gileadi?” Yehoshafati akamjibu hivi mfalme wa Israeli: “Mimi ni kama wewe. Watu wangu ni kama watu wako. Farasi wangu ni kama farasi wako.”^d

5 Lakini Yehoshafati akamwambia mfalme wa Israeli: “Tafadhali, kwanza tafuta^e neno la Yehova.”^f **6** Kwa hiyo mfalme wa Israeli akawakusanya pamoja manabii, wanau-me wapatao 400, akawauliza: “Je, niende kupigana vita dhidi ya Ramothi-gileadi, au ni-siende?” Wakasema: “Panda uende, na Yehova atalitia jiji hilo mikononi mwako.”

7 Kisha Yehoshafati akasema: “Je, hakuna nabii wa Yehova mahali hapa? Acheni tumuulize yeye pia.”^g **8** Ndipo mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: “Bado kuna mtu mmoja ambaye tunaweza kumwomba ushauri kutoka kwa Yehova;^h lakini ninamchukia,ⁱ kwa maana hatabiri kamwe mambo mema kunihusu, ila mabaya tu./ Anaitwa Mikaya mwana wa Imla.” Hata hivyo, Yehoshafati akasema: “Mfalme, usiseme jambo kama hilo.”

9 Basi mfalme wa Israeli akamwita ofisa fulani wa

SURA YA 22

a 1Fa 15:24

b 2Nya 18:2, 3

c Yos 20:8, 9
1Fa 4:7, 13d 2Fa 3:7
2Nya 19:2

e Hes 27:21

f 2Nya 18:4, 5

g 2Fa 3:11
2Nya 18:6, 7

h 1Fa 18:4

i 1Fa 21:20
2Nya 36:16j Isa 30:9, 10
Yer 38:4

Safu ya 2

a 2Nya 18:8-11

b Eze 13:2, 3

c 2Nya 18:12-16

makao ya mfalme na kumwambia: “Mlete haraka Mikaya mwana wa Imla.”^a

10 Sasa mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda walikuwa wameketi kila mmoja wao kwenye kiti chake cha ufalme, akiwa amevaa mavazi ya kifalme, katika uwanja wa kupuria nafaka kwenye lango la kuingia Samaria, na manabii wote walikuwa wakitabiri mbele yao.^b **11** Kisha Sedekia mwana wa Kenaana akajitengenezea pembe za chuma na kusema: “Yehova anasema hivi: ‘Kwa pembe hizi utawapiga* Wasiria mpaka utakopowaangamiza.’” **12** Wale manabii wengine wote walikuwa wakitabiri vivyo hivyo, wakisema: “Panda mpaka Ramothi-gileadi, nawe utafanikiwa; Yehova atalitia jiji hilo mikononi mwako mfalme.”

13 Basi mjumbe aliyenda kumwita Mikaya akamwambia: “Tazama! Manabii wote kwa pamoja wanasema mema kumhusu mfalme. Tafadhali, acha neno lako liwe kama maneno yao, useme mema.”^c

14 Lakini Mikaya akasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, jambo lolote ambalo Yehova ataniambia ndilo nitakalosema.” **15** Kisha akaingia kwa mfalme, naye mfalme akamuuliza: “Mikaya, je, twende kupigana vita dhidi ya Ramothi-gileadi, au tusiende?” Mara moja akajibu: “Panda uende nawe utafanikiwa; Yehova atalitia jiji hilo mikononi mwako.” **16** Ndipo mfalme akamuuliza: “Nitakuapisha mara ngapi kwamba hupaswi kuniambia

22:11 *Au “utawasukuma.”

jambo lingine lolote isipokuwa ukweli katika jina la Yehova?" **17** Basi Mikaya akasema: "Ninawaona Waisraeli wote wakiwa wametawanyika milimani,^a kama kondoo wasio na mchungaji. Yehova akasema: 'Hawa hawana bwana. Acha kila mmoja wao arudi kwa amani nyumbani kwake.'"

18 Kisha mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: "Je, sikukwambia, 'Hatatabiri mambo mema kunihusu, ila mabaya?'"^b

19 Ndipo Mikaya akasema: "Basi, sikia neno la Yehova: Nilimwona Yehova akiwa ameketi kwenye kiti chake cha ufalme^c na jeshi lote la mbinguni likiwa limesimama kando yake, upande wake wa kulia na upande wake wa kushoto.^d **20** Hala fu Yehova akauliza, 'Ni nani atakayemdanganya Ahabu, ili apande kwenda na kufia huko Ramothi-gileadi?' Na malaika mmoja akasema jambo moja na mwingine akasema jambo lingine. **21** Kisha roho^{*e} fulani akaja na kusimama mbele za Yehova na kusema, 'Mimi nitamdanganya.' Yehova akamuuliza, 'Utatumia njia gani?' **22** Akajibu, 'Nitaenda na kuwa roho ya udanganyifu katika vinywa vya manabii wake wote.'^f Kwa hiyo akasema, 'Utamdanganya, na zaidi ya hilo, utafanikiwa. Nenda ukafanye hivyo.' **23** Na sasa Yehova ametia roho ya udanganyifu katika vinywa vya hawa manabii wako wote,^g lakini Yehova ametangaza kwamba utapata msiba."^h

22:21 *Au "malaika."

SURA YA 22

a Kum 28:15, 25

b 2Nya 18:17

c Isa 6:1
Eze 1:26

d 2Nya 18:18-22
Ayu 1:6
Da 7:9, 10
Mt 18:10
Ufu 5:11

e Zb 104:4
Ebr 1:7, 14

f 1Fa 22:6

g Eze 14:9

h 1Fa 20:42

Safu ya 2

a 2Nya 18:23-27

b Ebr 11:32, 36

c Hes 16:28, 29

d 2Nya 18:28-32

e 2Nya 35:22

f 1Fa 20:1

24 Sasa Sedekia mwana wa Kenaana akamkaribia Mikaya na kumpiga kwenye shavu na kumuuliza: "Roho ya Yehova iliniacha jinsi gani na kuja kuzungumza nawe?"^a **25** Mikaya akajibu: "Tazama! Utajua ni jinsi gani utakapoiingia katika chumba cha ndani zaidi kujificha." **26** Ndipo mfalme wa Israeli akasema: "Mchukue Mikaya umpeleke kwa Amoni mkuu wa jiji na kwa Yoashi mwana wa mfalme. **27** Waambie, 'Mfalme anasema hivi: 'Mfungeni mtu huyu gerezani^b na kumlisha kiasi kidogo cha mkate na maji mpaaka nitakaporudi kwa amani.'"^c **28** Lakini Mikaya akasema: "Ukirudi kwa amani, basi Yehova hajazungumza nami."^c Kisha akasema: "Zingatieni maneno yangu, enyi watu wote."

29 Basi mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda wakapanda kwenda Ramothi-gileadi.^d **30** Ndipo mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: "Nitabadi-li sura yangu na kuingia vitani, lakini wewe vaa mavazi yako ya kifalme." Kwa hiyo mfalme wa Israeli akabadi-li sura yake^e na kuingia vitani. **31** Sasa mfalme wa Siria alikuwa amewaagiza hivi makamanda wake 32 wa magari ya vita:^f "Mspigane na yeyote, mdogo au mkubwa, isipokuwa mfalme wa Israeli." **32** Na mara tu makamanda hao wa magari ya vita walipomwona Yehoshafati, wakambiana: "Hakika huyu ndiye mfalme wa Israeli." Basi wakameukia ili kupigana naye; na Yehoshafati akaanza kulilia msaada. **33** Makamanda hao

wa magari ya vita walipoona kwamba hakuwa mfalme wa Israeli, mara moja wakaacha kumfuatia.

34 Lakini mtu fulani alivuta upinde wake bila kukusudia na kumpiga mfalme wa Israeli katikati ya sehemu ambazo koti lake la vita linaungana. Basi mfalme akamwambia mtu aliyeendesha gari lake: "Geuka uniondoe vitani,* kwa sababu nimejeruhiwa vibaya."^a

35 Vita vikapamba moto siku hiyo yote, nao wakalazimika kumsimamisha mfalme ndani ya gari akiwaelekea Wasiria. Damu ya jeraha lake ikamwagika ndani ya gari lake la vita, akafa jioni.^b **36** Jua lilipokuwa likitua amri hii ikatanzwa kambini: "Kila mtu aende katika jiji lake! Kila mtu aende katika nchi yake!"^c **37** Basi mfalme akafa, akaletwa Samaria; wakamzika mfalme huko Samaria. **38** Walipolisafisha gari hilo la vita kando ya kidi-mbwi cha Samaria, mbwa waliramba damu yake na makahaba wakaogea mahali hapo,* kama Yehova alivyokuwa amesema.^d

39 Na mambo mengine katika historia ya Ahabu, mambo yote aliyofanya na nyumba aliyojenga ya* pembe za tembo^e na majiji yote aliyojenga, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **40** Kisha Ahabu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake;^f na Ahazia^g mwana wake akawa mfalme baada yake.

22:34 *Tnn., "kambini." **22:38** *Au labda, "mbwa waliramba damu yake mahali ambapo makahaba waliogea." **22:39** *Au "jumba la mfalme alilojenga la."

SURA YA 22

a 2Nya 18:33, 34

b 1Fa 20:42

c 1Fa 22:17

d 1Fa 21:18, 19

e 1Fa 10:22
Eze 27:15

f 1Fa 16:28

g 2Fa 1:2
2Nya 20:35

Safu ya 2

a 1Nya 3:10
2Nya 17:1
2Nya 20:31
Mt 1:8b 1Fa 15:11
2Nya 14:11
2Nya 15:8

c 2Nya 17:3

d Kum 12:14
1Fa 14:23
1Fa 15:14e 2Nya 18:1
2Nya 19:2f Kum 23:17, 18
1Fa 14:24

g 1Fa 15:11, 12

h Mwa 36:1, 9

i 2Sa 8:14
2Fa 8:20-22
Zb 108:9

j 1Fa 10:22

k 1Fa 9:26
2Nya 20:35-37

41 Yehoshafati^a mwana wa Asa aliwekwa kuwa mfalme wa Yuda katika mwaka wa nne wa utawala wa Mfalme Ahabu wa Israeli. **42** Yehoshafati alikuwa na umri wa miaka 35 alipowekwa kuwa mfalme, naye alitawala kwa miaka 25 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Azuba binti ya Shilhi. **43** Yehoshafati aliendelea kutembea katika njia yote ya Asa^b baba yake. Hakugeuka na kuiacha njia hiyo, naye alitenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova.^c Hata hivyo, mahali pa juu hapakuondolewa, na bado watu walikuwa wakitoa dhabihu na kufukiza moshi wa dhabihu mahali pa juu.^d **44** Yehoshafati alidumisha mahusiano ya amani na mfalme wa Israeli.^e **45** Na mambo mengine katika historia ya Yehoshafati, mambo makuu aliyotekeleza na jinsi alivyopigana vita, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **46** Pia aliwaondoa kabisa nchini wanaume wote makahaba wa hekaluni^f waliobaki katika siku za Asa baba yake.^g

47 Wakati huo hakukuwa na mfalme katika nchi ya Edomu;^h naibu ndiye aliyetawala kama mfalme.ⁱ

48 Yehoshafati pia akategeneza meli* za Tarshishi za kwenda Ofiri kuleta dhahabu,^j lakini hazikwenda kwa sababu meli hizo zilivunjika huko Esion-geberi.^k **49** Wakati huo ndipo Ahazia mwana wa Ahabu alipomwambia Yehoshafati: "Waruhusu watumishi wangu wasafiri na watumishi wako katika meli

22:48 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

hizo,” lakini Yehoshafati haku-kubali.

50 Kisha Yehoshafati akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake^a katika Jiji la Daudi babu yake; na Yehoram^b mwanawe akawa mfalme baada yake.

51 Ahazia^c mwana wa Ahabu akawa mfalme wa Israeli huko Samaria katika mwaka wa 17 wa utawala wa Mfalme Yehoshafati wa Yuda, naye alitawala Israeli kwa miaka

SURA YA 22

a 1Fa 2:10

b 2Fa 8:16

2Nya 21:1, 5

c 2Fa 1:2

Safu ya 2

a 1Fa 16:30

b 1Fa 21:25

c 1Fa 12:28-30

1Fa 13:33

d 1Fa 16:31, 32

2Fa 1:2

e Kut 20:3

Kut 34:14

miwili. **52** Aliendelea kute-nda maovu machoni pa Yehova na kutembea katika njia ya baba yake^a na mama yake^b na katika njia ya Yeroboamu mwana wa Nebati, aliyesababisha Waisraeli watende dhambi.^c **53** Aliendelea kumwabu Baali^d na kumwinamia, akaendelea kumkasirisha Yehova Mungu wa Israeli,^e kama baba yake alivyokuwa amefanya.

KITABU CHA PILI CHA

WAFALME

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Eliya atabiri kifo cha Ahazia (1-18)</p> <p>2 Eliya apelekwa juu katika dhoruba ya upepo (1-18)
Elisha apata vazi rasmi la Eliya (13, 14)
Elisha ayaponya maji ya Yeriko (19-22)
Dubu wawaua wavulana kutoka Betheli (23-25)</p> <p>3 Yehoram, mfalme wa Israeli (1-3)
Wamoabu wawaasi Waisraeli (4-25)
Wamoabu washindwa (26, 27)</p> <p>4 Elisha afanya mafuta ya mjane yaongezeke (1-7)
Ukarimu wa mwanamke Mshunamu (8-16)
Mwanamke huyo athawabishwa kwa kupewa mwana; mwana huyo afa (17-31)
Elisha amfufua mwana huyo (32-37)
Elisha aufanya mchuzi unyweke (38-41)
Elisha afanya mikate iongezeke (42-44)</p> <p>5 Elisha amponya Naamani ukoma (1-19)
Gehazi mwenye pupa apigwa na ukoma (20-27)</p> <p>6 Elisha afanya shoka lielee (1-7)</p> | <p>Elisha apambana na Wasiria (8-23)
Macho ya mtumishi wa Elisha yafunguliwa (16, 17)
Wasiria yafunguliwa akili (18, 19)
Njaa kali katika jiji lililozingirwa la Samaria (24-33)</p> <p>7 Elisha atabiri mwisho wa njaa kali (1, 2)
Chakula chatikana katika kambi iliyoachwa ya Wasiria (3-15)
Unabii wa Elisha watimizwa (16-20)</p> <p>8 Mwanamke Mshunamu arudishiwa shamba lake (1-6)
Elisha, Ben-hadadi, na Hazaeli (7-15)
Yehoram, mfalme wa Yuda (16-24)
Ahazia, mfalme wa Yuda (25-29)</p> <p>9 Yehu atiwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli (1-13)
Yehu amua Yehoram na Ahazia (14-29)
Yezebeli auawa; mbwa wala maiti yake (30-37)</p> <p>10 Yehu awaua watu wa nyumba ya Ahabu (1-17)
Yehonadabu ajiunga na Yehu (15-17)
Yehu awaua waabudu wa Baali (18-27)</p> |
|--|--|

- Maelezo kuhusu utawala wa Yehu (28-36)
- 11 Athalia aunyakua ufalme (1-3)
Yehoashi awekwa kisiri kuwa mfalme (4-12)
Athalia auawa (13-16)
Mabadiliko yaliyofanywa na Yehoyada (17-21)
- 12 Yehoashi, mfalme wa Yuda (1-3)
Yehoashi arekebisha hekalu (4-16)
Wasiria wavamia (17, 18)
Yehoashi auawa (19-21)
- 13 Yehoahazi, mfalme wa Israeli (1-9)
Yehoashi, mfalme wa Israeli (10-13)
Elisha apima bidii ya Yehoashi (14-19)
Kifo cha Elisha; mifupa yake yamfufua mtu (20, 21)
Unabii wa mwisho wa Elisha watimizwa (22-25)
- 14 Amazia, mfalme wa Yuda (1-6)
Apigana vita na Waedomu na Waisraeli (7-14)
Kifo cha Yehoashi wa Israeli (15, 16)
Kifo cha Amazia (17-22)
Yeroboamu wa Pili, mfalme wa Israeli (23-29)
- 15 Azaria, mfalme wa Yuda (1-7)
Wafalme wa mwisho wa Israeli: Zekaria (8-12), Shalumu (13-16), Menahemu (17-22), Pekahia (23-26), Peka (27-31)
Yothamu, mfalme wa Yuda (32-38)
- 16 Ahazi, mfalme wa Yuda (1-6)
Ahazi awahonga Waashuru (7-9)
Ahazi aiga madhabahu ya wapagani (10-18)
Kifo cha Ahazi (19, 20)
- 17 Hoshea, mfalme wa Israeli (1-4)
Kuanguka kwa Israeli (5, 6)
Waisraeli wapelekwa uhamishoni kwa sababu ya uasi imani (7-23)
Wageni waletwa katika majiji ya Samaria (24-26)
Mchanganyiko wa dini katika Samaria (27-41)
- 18 Hezekia, mfalme wa Yuda (1-8)
Maelezo kuhusu kuanguka kwa Israeli (9-12)
Senakeribu avamia Yuda (13-18)
- Rabshake amdhihaki Yehova (19-37)
- 19 Hezekia amwomba Mungu msaada kupitia Isaya (1-7)
Senakeribu alitisha jiji la Yerusalemu (8-13)
Sala ya Hezekia (14-19)
Isaya ampa Hezekia jibu kutoka kwa Mungu (20-34)
Malaika awaua Waashuru 185,000 (35-37)
- 20 Hezekia awa mgonjwa kisha apona (11-11)
Wajumbe kutoka Babiloni (12-19)
Kifo cha Hezekia (20, 21)
- 21 Manase, mfalme wa Yuda; jinsi alivyomwaga damu (1-18)
Jiji la Yerusalemu kuharibiwa (12-15)
Amoni, mfalme wa Yuda (19-26)
- 22 Yosia, mfalme wa Yuda (1, 2)
Maagizo ya kurekebisha hekalu (3-7)
Kitabu cha Sheria chapatikana (8-13)
Hulda atabiri msiba (14-20)
- 23 Yosia afanya mabadiliko (1-20)
Pasaka yasherehekewa (21-23)
Yosia afanya mabadiliko zaidi (24-27)
Kifo cha Yosia (28-30)
Yehoahazi, mfalme wa Yuda (31-33)
Yehoyakimu, mfalme wa Yuda (34-37)
- 24 Uasi na kifo cha Yehoyakimu (1-7)
Yehoyakini, mfalme wa Yuda (8, 9)
Uhamisho wa kwanza wa kwenda Babiloni (10-17)
Sedekia, mfalme wa Yuda; uasi wake (18-20)
- 25 Nebukadneza azingira Yerusalemu (1-7)
Jiji la Yerusalemu laharibiwa pamoja na hekalu lake; uhamisho wa pili (8-21)
Gedalia awekwa kuwa gavana (22-24)
Gedalia auawa; watu wakimbilia Misri (25, 26)
Yehoyakini aachiliwa huru Babiloni (27-30)

1 Baada ya kifo cha Ahabu, Wamoabu^a waliwaasi Waisraeli.

2 Huo ndio wakati ambapo Ahazia alianguka chini kupitia kiunzi kilichokuwa katika chumba chake cha darini kule Samaria, akajeruhiwa. Kwa hiyo akawatuma wajumbe, akawaambia: “Nendeni mkaumuulize Baal-zebubu mungu wa Ekroni^b ikiwa nitapona jeraha hili.”^c **3** Lakini malaika wa Yehova akamwambia Eliya*^d Mtishbi: “Ondoka, nenda ukakutane na wajumbe wa mfalme wa Samaria, uwaulize, ‘Je, mnaenda kutafuta ushauri kutoka kwa Baal-zebubu mungu wa Ekroni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli?’” **4** Kwa hiyo Yehova anasema hivi: “Hutatoka katika kitanda unacholalia, kwa maana hakika utakufa.”” Kisha Eliya akaenda zake.

5 Wajumbe hao waliporudi kwake, mara moja akawauliza: “Kwa nini mmerudi?” **6** Wakamjibu: “Kuna mtu aliyekuja kukutana nasi, akatuambia, ‘Nendeni, rudini kwa mfalme aliyewatuma mkamwambie, ‘Yehova anauliza hivi: ‘Je, unawatuma wajumbe waende kutafuta ushauri kutoka kwa Baal-zebubu mungu wa Ekroni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Kwa hiyo, hutatoka katika kitanda unacholalia, kwa maana hakika utakufa.’””^f **7** Ndipo mfalme akawauliza: “Mtu aliyekuja kukutana nanyi na kusema maneno hayo alikuwaje?” **8** Wakamwambia: “Alikuwa mwanaume aliyevaa vazi la manyo-

1:3 *Maana yake “Mungu Wangu Ni Yehova.”

SURA YA 1

a Mwa 19:36, 37
2Sa 8:2
Zb 60:8

b Yos 13:2, 3
1Sa 5:10

c 2Fa 1:16

d 1Fa 17:1
1Fa 18:36

e Isa 8:19
Yer 2:11

f 1Nya 10:13, 14

Safu ya 2

a 1Fa 19:19
Zek 13:4
Ebr 11:32, 37

b Mt 3:4

c Kum 33:1

d Hes 11:1
Hes 16:35
Lu 9:54
Yud 7

ya^a na mshipi wa ngozi kiunoni.”^b Mara moja akasema: “Ni Eliya Mtishbi.”

9 Kisha mfalme akamtuma mkuu wa 50 na wanaume wake 50 kwa Eliya. Mkuu huyo alipanda kwenda kumwona, akamkuta ameketi kwenye kilele cha mlima. Akamwambia: “Mtu wa Mungu wa kweli,^c mfalme anasema, ‘Shuka chini.’” **10** Lakini Eliya akamjibu mkuu huyo wa 50: “Ikiwa kwa kweli mimi ni mtu wa Mungu, moto na ushuke kutoka mbinguni,^d ukuteketeze wewe na wanaume wako 50.” Basi moto ukashuka kutoka mbinguni, ukamtekeza pamoja na wanaume wake 50.

11 Kwa hiyo mfalme akamtuma tena mkuu mwingine wa 50 na wanaume wake 50 kwenda kwa Eliya. Akaenda na kumwambia: “Mtu wa Mungu wa kweli, mfalme anasema, ‘Shuka chini haraka.’” **12** Lakini Eliya akawajibu, “Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu wa kweli, moto na ushuke kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na wanaume wako 50.” Basi moto wa Mungu ukashuka kutoka mbinguni, ukamtekeza pamoja na wanaume wake 50.

13 Kisha mfalme akamtuma tena mkuu wa tatu wa 50 na wanaume wake 50. Lakini yule mkuu wa tatu wa 50 akapanda, akainama na kupiga magoti mbele ya Eliya, akaanza kumsihi apate kibali mbele yake na kumwambia, “Mtu wa Mungu wa kweli, tafadhali, acha uhai wangu na uhai wa watumishi hawa wako 50 uwe* na thamani machoni

1:13 *Au “nafsi yangu na nafsi ya watumishi hawa wako 50 iwe.”

pako. **14** Tayari moto ume-shuka kutoka mbinguni ukawateketeza wale wakuu wawili wa kwanza wa 50 na makundi yao ya 50, lakini sasa acha uhai wangu uwe* na thamani machoni pako.”

15 Ndipo malaika wa Yehova akamwambia Eliya: “Shuka pamoja naye. Usimwogope.” Basi akainuka, akashuka na kwenda pamoja naye kwa mfalme. **16** Kisha Eliya akamwambia mfalme: “Yehova anasema hivi: ‘Uliwatuma wajumbe kutafuta ushuri kutoka kwa Baal-zebubu mungu wa Ekroni.^a Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli?’^b Kwa nini hukutafuta neno lake? Basi hutatoka katika kitanda unacholalia, kwa maana hakika utakufa.” **17** Kwa hiyo akafa, kulingana na neno la Yehova ambalo Eliya alikuwa amesema; na kwa kuwa Ahazia hakuwa na mwana, Yehoram^c akawa mfalme baada yake katika mwaka wa pili wa Yehoram^d mwana wa Yehoshafati mfalme wa Yuda.

18 Na mambo mengine katika historia ya Ahazia,^e mambo aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli?

2 Yehova alipokuwa karibu kumchukua Eliya^f kueleka mbinguni* katika dhoruba ya upepo,^g Eliya na Elisha^h wakaondoka Gilgali.ⁱ **2** Eliya akamwambia Elisha: “Kaa hapa, tafadhali, kwa sababu Yehova amenituma Betheli.” Lakini Elisha akasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kama unavyoi-

1:14 *Au “nafsi yangu iwe.” 1:17 *Yaa-ni, ndugu ya Ahazia. 2:1 *Au “angani.”

SURA YA 1

a Yos 13:2, 3

b 2Fa 1:3

c 2Fa 3:1
2Fa 9:22

d 2Fa 8:16

e 1Fa 22:51

SURA YA 2

f 1Fa 17:1

g 2Fa 2:11

h 1Fa 19:16

i 2Fa 4:38

Safu ya 2

a Mwa 28:18, 19
1Fa 12:28, 29
2Fa 2:23

b 1Fa 19:16

c Yos 6:26
1Fa 16:34

d 1Fa 19:19

e Kut 14:21, 22
Yos 3:17
2Fa 2:13, 14

shi,* sitakuacha.” Basi wakashuka kwenda Betheli.^a **3** Kisha wana wa manabii* huko Betheli wakaja kwa Elisha na kumuuliza: “Je, unajua kwamba leo Yehova anamchukua bwana wako asiwe kiongozi wako?”^b Ndipo akajibu: “Tayari najua. Nyamazeni.”

4 Sasa Eliya akamwambia: “Elisha, tafadhali kaa hapa, kwa sababu Yehova amenituma Yeriko.”^c Lakini Elisha akasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kama unavyoishi,* sitakuacha.” Basi wakaenda Yeriko. **5** Kisha wana wa manabii waliokuwa Yeriko wakaenda kwa Elisha na kumuuliza: “Je, unajua kwamba leo Yehova anamchukua bwana wako asiwe kiongozi juu yako?” Ndipo akajibu: “Tayari najua. Nyamazeni.”

6 Sasa Eliya akamwambia: “Kaa hapa, tafadhali, kwa sababu Yehova amenituma Yordani.” Lakini Elisha akasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kama unavyoishi,* sitakuacha.” Basi wote wawili wakaendelea na safari. **7** Na wana 50 wa manabii wakaenda pia, wakasimama na kuwatazama kwa mbali wote wawili wakiwa wamesimama kando ya Mto Yordani. **8** Kisha Eliya akachukua vazi lake rasmi,^d akaliviringa na kuyapiga maji, nayo yakagawanyika kushoto na kulia, basi wote wawili wakavuka ng’ambo kupitia nchi kavu.^e

9 Mara tu walipovuka, Eliya akamwambia Elisha:

2:2, 4, 6 *Au “nafsi yako inavyoishi.” 2:3 *Inaonekana maneno “wana wa manabii” yanarejelea shule ya kuwafundisha manabii au chama cha manabii.

“Omba jambo unalotaka nikutendee kabla sijachukuliwa na kukuacha.” Basi Elisha akamuuliza: “Tafadhali, naweza kupata mafungu mawili^a ya * roho yako?”^b **10** Eliya akajibu: “Umeomba jambo gumu. Ikiwa utaniona nitakapochukuliwa na kukuacha, itakuwa hivyo kwako; lakini usiponiona, jambo hilo halitatokea.”

11 Walipokuwa wakitembea, huku wakizungumza, kwa ghafla gari la moto na farasi wa moto^c wakawatangani-sha, na Eliya akapanda kuelekea mbinguni* katika dhoruba ya upepo.^d **12** Elisha alitazama huku akipaza sauti, “Baba yangu, baba yangu! Gari la Israeli na wapanda farasi wake!”^e Alipotoweka kabisa machoni pake, akashika mavazi yake mwenyewe na kuyararua vipande viwili.^f **13** Ndipo akaliokota vazi rasmi^g la Eliya lililokuwa limeanguka kutoka kwa Eliya, akarudi na kusimama kwenye ukingo wa Yordani. **14** Kisha akachukua vazi rasmi la Eliya lililokuwa limeanguka kutoka kwake, akayapiga maji na kuuliza: “Yuko wapi Yehova, Mungu wa Eliya?” Alipoyapiga maji, yaligawanyika kushoto na kulia, Elisha akavuka ng’ambo.^h

15 Wana wa manabii waliokuwa Yeriko walipomwona kwa mbali, wakasema: “Roho ya Eliya imetua juu ya Elisha.”ⁱ Basi wakaenda kukutana naye na kumwinamia mpaka ardhini. **16** Wakamwambia: “Hapa sisi watumishi wako tuna wanaume mashujaa 50. Tafadhali, waruhusu waende

2:9 *Au “sehemu mbili za.” 2:11 *Au “angani.”

SURA YA 2

a Kum 21:17

b Kum 34:9
1Fa 19:16
Lu 1:17c 2Fa 6:17
Zb 68:17d 2Nya 21:5, 12
Yoh 3:13

e 2Fa 13:14

f 2Sa 1:11, 12
Ayu 1:19, 20g 1Fa 19:19
2Fa 1:8
Zek 13:4
Mt 3:4h Yos 3:13
2Fa 2:8i Hes 11:24, 25
Hes 27:18, 20
2Fa 2:9

Safu ya 2

a 1Fa 18:11, 12

b Yos 6:26
1Fa 16:34

c Kum 34:1-3

d Kut 15:23-25
2Fa 4:38-41e 2Nya 36:15, 16
Lu 10:16

f Met 17:12

kumtafuta bwana wako. Labda roho ya* Yehova imemwina juu na kumtupa juu ya mojawapo ya milima au katika mojawapo ya mabonde.”^a Lakini akawaambia: “Msiwatumeme.” **17** Hata hivyo, waliendelea kumsihi mpaka akaona aibu, kwa hiyo akasema: “Watumeni.” Wakawatuma wanaume 50, nao wakaendelea kumtafuta kwa siku tatu, lakini hawakumpata. **18** Waliporudi kwake, alikuwa anakaa Yeriko.^b Kisha akawauliza: “Je, sikuwaambia msiende?”

19 Baada ya muda watu wa jiji hilo wakamwambia Elisha: “Bwana wetu, unaona kwamba jiji hili liko mahali pazuri;^c lakini maji ni mabaya, na wakaaji wa nchi ni tasa.”* **20** Akawaambia: “Nileteeini bakuli dogo jipya, mweke chumvi ndani yake.” Basi wakamletea. **21** Kisha akatoka na kwenda kwenye chemchemi ya maji hayo, akatupa chumvi ndani yake^d na kusema: “Yehova anasema hivi: ‘Nimeyaponya maji haya. Hayatasababisha tena kifo wala utasa.’”*

22 Na maji hayo yameponywa mpaka leo hii, kulingana na neno alilosema Elisha.

23 Akapanda kutoka huko na kwenda Betheli. Alipokuwa akitembea njiani, wavulana fulani walitoka jijini na kuanza kumdhihaki,^e wakaendelea kumwambia: “Panda juu, wewe mwenye upara! Panda juu, wewe mwenye upara!” **24** Hatimaye akageuka na kwatazama, akawalaani katika jina la Yehova. Ndipo dubu jike wawili^f wakatoka msitu-

2:16 *Au “upepo wa.” 2:19 *Au labda, “yanaharibu mimba.” 2:21 *Au labda, “kuharibu mimba.”

ni na kuwararua vipandevipande watoto 42.^a **25** Kuto ka huko, akaendelea na safari mpaka Mlima Karmeli,^b na kutoka huko akarudi Samaria.

3 Yehoram^c mwana wa Ahabu akawa mfalme wa Israeli kule Samaria katika mwaka wa 18 wa utawala wa Mfalme Yehoshafati wa Yuda, naye alitawala kwa miaka 12. **2** Akaendelea kute nda maovu machoni pa Yehova, lakini si kwa kadiri aliyotenda baba yake au mama yake, kwa maana aliondoa nguzo takatifu ya Baali ambayo baba yake alikuwa ametengeneza.^d **3** Hata hivyo, alishikamana na dhambi ambazo Yeroboamu mwana wa Nebati alikuwa amesababisha Waisraeli watende.^e Hakuziacha.

4 Mesha mfalme wa Moabu alikuwa mfuaji wa kondoo, naye alikuwa akilipa wanakondoo 100,000 na kondoo dume 100,000 ambao hawajakatwa manyoya kama ushuru kwa mfalme wa Israeli. **5** Mara tu Ahabu alipokufa,^f mfalme wa Moabu akamwasi mfalme wa Israeli.^g **6** Basi Mfalme Yehoram akaondoka Samaria siku hiyo na kuwakusanya Waisraeli wote. **7** Akamtumia pia ujumbe Mfalme Yehoshafati wa Yuda, akisema: "Mfalme wa Moabu ameniasi. Je, utienda pamoja nami kupigana vita dhidi ya Moabu?" Akasema: "Nitaenda.^h Mimi ni kama wewe. Watu wangu ni kama watu wako. Farasi wangu ni kama farasi wako."ⁱ **8** Kisha akamuuliza: "Tupande kupitia njia gani?" Akajibu: "Kupitia njia ya nyika ya Edomu."

9 Basi mfalme wa Israeli akaondoka pamoja na mfalme

SURA YA 2

a 2Fa 1:10

b 2Fa 4:25

SURA YA 3

c 2Fa 1:17

d 1Fa 16:30-33

e 1Fa 12:28-30

f 1Fa 22:37

g 2Sa 8:2

h 2Nya 19:2

i 1Fa 22:3, 4

Safu ya 2

a 2Sa 8:14

b 1Fa 22:7

c 1Fa 19:16
2Fa 2:15

d 1Fa 19:19, 21

e 1Sa 2:30
Eze 14:3

f Amu 10:14
1Fa 18:19
1Fa 22:6

g 2Nya 17:3, 4
2Nya 19:3, 4

h Met 15:29

i 1Sa 10:5
1Nya 25:1

wa Yuda na mfalme wa Edomu.^a Baada ya kuzunguka kwa siku saba, jeshi na wanyama wa kufugwa waliokuwa wakifafuata hawakuwa na maji.

10 Mfalme wa Israeli akasema: "Inasikitisha sana! Yehova ametuita sisi wafalme watatu ili tu atutie mikononi mwa Moabu!" **11** Ndipo Yehoshafati akauliza: "Je, hakuna nabii wa Yehova mahali hapa ambaye tunaweza kumwomba ushauri kutoka kwa Yehova?"^b Basi mmoja wa watumishi wa mfalme wa Israeli akajibu: "Yupo Elisha^c mwana wa Shafati, aliyekuwa aki mmiminia Eliya maji mikononi."^{*d} **12** Kisha Yehoshafati akasema: "Neno la Yehova liko pamoja naye." Basi mfalme wa Israeli na pia Yehoshafati na mfalme wa Edomu wakashuka kwenda kumwona.

13 Elisha akamwambia mfalme wa Israeli: "Kwa nini ume kuja kuniona?"^{*e} Nenda kwa manabii wa baba yako na kwa manabii wa mama yako."^f Lakini mfalme wa Israeli akamwambia: "Sitaenda, kwa maana ni Yehova aliyetuita sisi wafalme watatu ili atutie mikononi mwa Moabu." **14** Elisha akamwambia: "Kwa hakika kama anavyoishi Yehova wa majeshi ambaye ninamtumikia,^{*} kama singekuwa ninamheshimu Mfalme Yehoshafati^g wa Yuda, singekutazama wala kukutilia maanani.^h **15** Sasa niletee mpiga kinubi."^{*i} Mara

3:11 *Au "aliyekuwa mtumishi wa Eliya." **3:13** *Tnn., "Kuna nini kati yangu nawe?" **3:14** *Tnn., "ambaye ninasimama mbele zake." **3:15** *Au "mwana-muziki."

tu mpiga kinubi huyo alipoanza kupiga kinubi, mkono wa Yehova ukaja juu ya Elisha.^a

16 Akasema, “Yehova anasema hivi: ‘Chimbeni mitaro katika bonde* hili, **17** kwa maana Yehova anasema hivi: ‘Hamtaona upepo, wala hamtaona mvua; hata hivyo bonde* hili litajaa maji,^b nanyi mtakunywa maji yake, ninyi, ng’ombe wenu, na wanyama wenu wengine.”’ **18** Lakini hili ni jambo dogo sana machoni pa Yehova,^c kwa maana ataitia pia Moabu mikononi mwenu.^d **19** Mnapaswa kuangamiza kila jiji lenye ngome^e na kila jiji bora, mnapaswa kuukata kila mti mzuri, mnapaswa kuziba chemchemi zote za maji, nanyi mnapaswa kuharibu kila shamba zuri kwa kutupa mawe humo.”^f

20 Na asubuhi, wakati ambapo toleo la nafaka la asubuhi hutolewa,^g maji yakaanza kuja kwa ghafla kutoka upande wa Edomu, na nchi ikajaa maji.

21 Wamoabu wote wakasi-
kia kwamba wafalme hao walikuwa wamekuja kupigana nao, basi wakawakusanya pamoja wanaume wote walioweza kubeba silaha,* nao wakasimama mpakani. **22** Wali-poamka asubuhi na mapema, jua lilikuwa likiangaza juu ya maji, na Wamoabu waliokuwa upande wa pili waliona maji yakiwa mekundu kama damu. **23** Wakasema: “Hii ni damu! Hakika wafalme wamechinjana wenyewe kwa upanga. Haya basi, enyi Wamoabu, twendeni tukachukue nyara!”^h **24** Walipoingia katika kambi

3:16, 17 *Au “korongo.” 3:21 *Au “wote waliojifunga mshipi.”

SURA YA 3

a 1Fa 18:46
Eze 1:3
Mdo 11:21

b Zb 107:35

c Yer 32:17
Mk 10:27

d Kum 28:7

e Kum 3:5

f 2Fa 3:25

g Kut 29:39, 40

h Kut 15:9, 10

Safu ya 2

a Law 26:7

b Mwa 26:15
2Nya 32:4

c 2Fa 3:19

d Isa 16:7

e 2Fa 3:9

f Kum 12:31
2Nya 28:1, 3
Zb 106:37, 38

SURA YA 4

g 2Fa 2:3, 5

h 1Fa 19:18

ya Israeli, Waisraeli wakatoka na kuanza kuwaua Wamoabu, nao wakawakimbia.^a Waisraeli wakazidi kuingia Moabu, wakawaua Wamoabu kadiri wali-vyosonga. **25** Wakabomoa majiji, na kila mtu akatupa jiwe katika kila shamba zuri, na kulijaza mawe; wakaziba kila chemchemi ya maji^b na kuukata kila mti mzuri.^c Mwishowe ni kuta za mawe za jiji la Kir-haresethi^d pekee zilizobaki, na watu wenye makombeo wakalizunguka na kulia-ngamiza.

26 Mfalme wa Moabu alipoona kwamba ameshindwa vitani, akachukua wanaume 700 waliojihami kwa mapanga ili wapenye na kuingia kwa mfalme wa Edomu;^e lakini hawakuweza. **27** Basi akamchukua mwana wake mzaliwa wa kwanza ambaye angetawala baada yake akamtoa kuwa dhabihu ya kutekelezwa^f juu ya ukuta. Wamoabu wakawa na ghadhabu kali dhidi ya Waisraeli, kwa hiyo Waisraeli wakaacha kumshambulia mfalme huyo na kurudi katika nchi yao.

4 Basi mke wa mmoja wa wana wa manabii^g akamlilia Elisha akisema: “Mume wangu ambaye ni mtumishi wako amekufa, nawe unajua vizuri kwamba mtumishi wako alimwogopa Yehova sikuzote.^h Sasa mtu fulani aliyem dai mume wangu deni fulani amekuja kuwachukua watoto wangu wawili wawe watumwa wake.” **2** Kwa hiyo Elisha akamuuliza: “Nikusaidieje? Niambiye, una nini nyumbani?” Akajibu: “Mimi kijakazi wako sina chochote

nyumbani ila mtungi wa mafuta.”^a **3** Basi Elisha akamwambia: “Nenda nje, wao mbe majirani wako wote vyombo, vyombo vitupu. Usiombe vyombo vichache. **4** Kisha uingie nyumbani mwako pamoja na wanao na kufunga mlango. Jaza vyombo hivyo vyote, na uweke kando vilivyojaa.” **5** Basi mwanamke huyo akaenda zake.

Alipoingia nyumbani pamoja na wanawe na kufunga mlango, wakamletea vyombo, naye akaendelea kuvijaza mafuta.^b **6** Vyombo hivyo vilipojaa, akamwambia hivi mmoja wa wanawe: “Nilettee chombo kingine.”^c Lakini mwana huyo akamwambia: “Hakuna vyombo vingine.” Basi mafuta yakakoma.^d **7** Kwa hiyo mwanamke huyo akaenda kwa yule mtu wa Mungu wa kweli, mtu huyo akamwambia: “Nenda, yauze mafuta hayo ulipe madeni yako, nawe pamoja na wanao mna-weza kuishi kwa kile kinachobaki.”

8 Siku moja Elisha alienda Shunemu,^e na huko kulikuwa na mwanamke mmoja maarufu, mwanamke huyo akamsihi sana ale chakula huko.^f Na kila mara alipopita mahali hapo, alikuwa akiingia mahali hapo kula chakula. **9** Basi mwanamke huyo akamwambia mume wake: “Najua kwamba mtu huyu anayepitia hapa kila mara ni mtu mtaakatifu wa Mungu. **10** Tafadhali, acha tutengeneze chumba kidogo juu ya paa,^g tumwekee humo kitanda, meza,

4:2 * Au “mtungi wa mafuta wenye mdomo wa birika.”

SURA YA 4

a 1Fa 17:9,12

b Mk 6:41
Mk 8:6-8
Yoh 2:7-9

c Mt 14:19

d Yos 5:12
1Fa 17:14

e Yos 19:17, 18

f Mwa 19:1-3
Amu 13:15g Amu 3:20
1Fa 17:19

Safu ya 2

a Mt 10:41
Ro 12:13
Ebr 13:2b 2Fa 5:25-27
2Fa 8:4

c Yos 19:17, 18

d Ro 16:6

e 2Fa 4:1, 2
Ebr 6:10

f 2Fa 8:3

g Mwa 15:2
Mwa 30:1

h Mwa 18:10

kiti, na kinara cha taa. Kisha, wakati wowote anapotutembelea, anaweza kukaa humo.”^a

11 Siku moja Elisha alifika huko, akaingia katika chumba hicho kilichokuwa paani ili alale. **12** Basi akamwambia Gehazi^b mtumishi wake: “Mwite huyo mwanamke Mshunamu.”^c Kwa hiyo akamwita, basi akaja na kusimama mbele yake. **13** Kisha Elisha akamwambia Gehazi: “Tafadhali mwambie mwanamke huyu, ‘Umejitaabisha sana kwa ajili yetu.’^d Tukufanyie nini?”^e Je, ninaweza kuzungumza na mfalme^f au mkuu wa jeshi kwa niaba yako?”^g Lakini mwanamke huyo akasema: “Ninaiishi miongoni mwa watu wangu mwenyewe.” **14** Kwa hiyo Elisha akauliza: “Basi tumfanyie nini mwanamke huyu?” Gehazi akasema: “Kwa kweli, hana mwana,^g na mume wake ni mzee.” **15** Mara moja akasema: “Mwite.” Basi akamwita, akaja na kusimama mlango ni. **16** Kisha Elisha akasema: “Wakati huu, mwaka ujao, utakuwa ukimkumbatia mwana.”^h Lakini mwanamke huyo akasema: “La hashu, bwana wangu, mtu wa Mungu wa kweli! Usindanganye mimi kijakazi wako.”

17 Hata hivyo, mwanamke huyo akapata mimba na kuzaa mwana wakati huohuo mwaka uliofuata, kama Elisha alivyo mwambia. **18** Mtoto huyo akakua, na siku moja alitoka kwenda kwa baba yake aliyekuwa na wavunaji. **19** Alikuwa akimwambia baba yake: “Kichwa changu kinauma, jamani kichwa changu kinauma!” Ndipo baba yake akamwambia mtumishi: “Mbebe umpeleke kwa mama yake.”

20 Basi akambeba na kumrudisha kwa mama yake, naye akakaa kwenye mapaja ya mama yake mpaka adhuri, kisha akafa.^a **21** Basi akapanda na kumlaza kwenye kitanda cha mtu wa Mungu wa kweli,^b akafunga mlango na kuondoka. **22** Sasa akamwita mume wake na kumwambia: “Tafadhali, mwagize mtumishi mmoja aje kwangu na punda mmoja, ili nie nde haraka kwa yule mtu wa Mungu wa kweli na kurudi.” **23** Lakini mume wake akasema: “Kwa nini unaenda kumwona leo? Si mwezi mpya^c wala sabato.” Hata hivyo, mwanamke huyo akasema: “Mambo yote yako sawa.” **24** Basi akaweka matandiko juu ya punda na kumwambia mtumishi wake: “Kaza mwendo. Usipunguze mwendo mpaka nitakapokwambia.”

25 Basi akaenda kwa mtu wa Mungu wa kweli kwenye Mlima Karmeli. Mara tu mtu wa Mungu wa kweli alipomwona kutoka mbali, akamwambia Gehazi mtumishi wake: “Tazama! Ndiye yule mwanamke Mshunamu anakuja. **26** Tafadhali, kimbia ukakutane naye na kumuuliza, ‘Je, u mzima? Je, mume wako ni mzima? Je, mtoto wako ni mzima?’” Mwanamke huyo akasema: “Mambo yote yako sawa.” **27** Mwanamke huyo alipofika kwa mtu wa Mungu wa kweli mlimani, mara moja akamshika miguu.^d Ndipo Gehazi akamkaribia ili amsukume mbali, lakini mtu wa Mungu wa kweli akasema: “Mwache, kwa maana ana* uchungu mwingi sana,

4:27 *Au “nafsi yake ina.”

SURA YA 4

a 1Fa 17:17

b 2Fa 4:9,10

c Hes 10:10
Hes 28:11

d Mt 28:9

Safu ya 2

a 2Fa 4:16

b 1Fa 18:46

c Mt 15:22, 28

d Mt 17:15, 16
Mk 9:17, 18

e 2Fa 4:21

f 1Fa 17:19, 20
Yoh 11:41
Mdo 9:40g 1Fa 17:21, 22
Mdo 20:9, 10

na Yehova amenificha jambo hilo na hajaniambia.” **28** Ndipo mwanamke huyo akasema: “Bwana wangu, je, nilikuomba mwana? Je, sikusema, ‘Usinipe tumaini la uwongo?’”^a

29 Mara moja akamwambia Gehazi: “Jifunge mavazi yako kiunoni,^b chukua fimbo yangu mkononi mwako, uende. Ukiutana na yeyote, usimsalimu; na yeyote akikusalimu, usimjibu. Nenda uiweke fimbo yangu juu ya uso wa mvulana huyo.” **30** Ndipo mama ya mvulana huyo akasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi na kama wewe mwenyewe unavyoishi,* sitakuacha.”^c Kwa hiyo Gehazi akaondoka na kwenda pamoja na mwanamke huyo. **31** Gehazi akawatangulia, akaiweka ile fimbo juu ya uso wa mvulana huyo, lakini hapakuwa na sauti yoyote wala dalili yoyote.^d Basi akarudi kukutana na Elisha na kumwambia: “Mvulana ha kuamka.”

32 Elisha alipoingia kati ka nyumba hiyo, mvulana huyo alikuwa amelala kwenye kitanda chake akiwa mfu.^e **33** Aliingia ndani, akajifungia humo pamoja na mvulana huyo na kuanza kusali kwa Yehova.^f **34** Kisha akapanda kitandani na kumlalia mtoto huyo, kinywa chake kikiwa juu ya kinywa cha mvulana huyo, macho yake juu ya macho yake, na viganja vyake juu ya viganja vyake, akaendelea kumlalia, na mwili wa mtoto huyo ukaanza kupata joto.^g

35 Kisha Elisha akatembea huku na kule chumbani, aka-

4:30 *Au “kama nafsi yako mwenyewe inavyoishi.”

panda kitandani na kumlalia tena. Mvulana huyo akapi-ga chafya mara saba, kisha akafungua macho.^a **36** Sasa akamwita Gehazi na kumwambia: "Mwite yule mwanamke Mshunamu." Basi akamwita, naye akaja. Ndipo Elisha akamwambia: "Mchukue mwanao."^b **37** Mwanamke huyo akaingia ndani, akaanguka miguuni pa Elisha na kuinama mbele yake mpaka ardhini, kisha akamchukua mwanawe na kutoka nje.

38 Elisha aliporudi Gilgali, kulikuwa na njaa kali nchini.^c Wana wa manabii^d walikuwa wameketi mbele yake, akamwambia mtumishi wake:^e "Weka kile chungu kikubwa motoni uwachemshie mchuzi wana wa manabii." **39** Basi mmoja wao akaenda shambani kuchuma miholi, akapata mزابيبو wa mwituni na kuchuma maboga ya mwituni kutoka kwenye mzabibu huo, akajaza vazi lake. Kisha akarudi na kuyakata vipandevipande ndani ya chungu cha mchuzi, bila kujua yalikuwa nini. **40** Baada ya wakawapakulia wanaume hao ili wale, lakini mara tu walipokunywa mchuzi huo, wakalia wakisema: "Kuna kifo ndani ya chungu hiki, Ee mtu wa Mungu wa kweli." Nao hawakuweza kuunywa. **41** Kwa hiyo Elisha akasema: "Leteni unga kidogo." Baada ya kuutupana ndani ya chungu hicho, akasema: "Wapakulieni watu." Na haku-kuwa tena na kitu chochote chenye kudhuru ndani ya chungu hicho.^f

42 Mtu fulani alikuja kutoka Baal-shalisha,^g akamletea mtu wa Mungu wa kweli mikate 20 ya shayiri^h iliyookwa kwa sha-

SURA YA 4

a 2Fa 8:1, 5

b Ebr 11:35

c Kum 28:23, 24
2Fa 8:1
Eze 14:13

d 2Fa 2:3, 5

e 2Fa 4:12

f Kut 15:23-25
2Fa 2:19-21

g 1Sa 9:3, 4

h Yoh 6:9

Safu ya 2

a 1Sa 9:6, 7

b Mt 14:17
Mk 8:4c Mt 14:20
Mk 8:8d Lu 9:17
Yoh 6:13

SURA YA 5

e 1Fa 19:16

f Mt 8:2
Mt 11:5
Lu 4:27

yiri iliyokomaa kwanza, pamoja na mfuko wa nafaka iliyo-toka kuvunwa.^a Kisha Elisha akasema: "Wape watu ili wale." **43** Hata hivyo, mtumishi wake akamuuliza: "Nitawezaje ku-wapa wanaume 100 chakula hiki?"^b Elisha akasema: "Wape watu ili wale, kwa maana Yehova anasema hivi: 'Watakula na kingine kitabaki.'"^c **44** Basi akawapa, nao wakala na kingine kikabaki,^d kama Yehova alivyosema.

5 Sasa Naamani, mkuu wa jeshi la mfalme wa Siria, alikuwa mtu maarufu aliyeheshimiwa na bwana wake, kwa sababu Yehova alikuwa amewapa Wasiria ushindi* kupitia yeye. Alikuwa shujaa hodari, ingawa alikuwa na ukoma.[#] **2** Pindi moja Wasiria walipovamia Israeli, walimchukua mateka msichana mdogo kutoka katika nchi ya Israeli, akawa kijakazi wa mke wa Naamani. **3** Msichana huyo alimwambia hivi bimbubwa wake: "Laiti bwana wangu angemtembelea nabii* aliye kule Samaria! Angemponya ukoma wake."^f **4** Basi akaenda* na kumwambia bwana wake mambo aliyosema msichana huyo kutoka Israeli.

5 Kisha mfalme wa Siria akasema: "Nenda sasa! Nami nitamtumia barua mfalme wa Israeli." Basi akaenda, akaondoka akiwa amebeba talanta kumi* za fedha, vipande 6,000 vya dhahabu, na mavazi kumi. **6** Akampelekea mfalme wa Israeli barua hiyo

5:1 *Au "wokovu." #Au "alikuwa na ugonjwa wa ngozi." 5:4 *Inawezekana ni Naamani. 5:5 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

ambayo ilisema hivi: “Pamoja na barua hii, ninamtu- ma mtumishi wangu Naamani ili umponye ukoma wake.” **7** Mara tu mfalme wa Israeli aliposoma barua hiyo, ali- yararua mavazi yake na kusema: “Je, mimi ni Mungu, ninaweza kuua na kumfanya mtu aende- lee kuwa hai?”^a Kwa maana ana- mtuma mtu huyu kwangu na kuniambia nimponye ukoma wake! Mnaona wenyewe kwa- mba anatafuta ugomvi nami.”

8 Lakini Elisha mtu wa Mu- ngu wa kweli aliposikia kwa- mba mfalme wa Israeli ame- yararua mavazi yake, mara moja akamtumia mfalme ujumbe huu: “Kwa nini uliyararua mavazi yako? Tafadhali, mru- husu aje kwangu ili ajue kwa- mba kuna nabii katika Israe- li.”^b **9** Basi Naamani akaja na farasi wake na magari yake ya vita, akasimama katika mlan- go wa nyumba ya Elisha. **10** Hata hivyo, Elisha aka- mtuma mjumbe amwambie: “Nenda ukaoge mara saba^c ka- tika Mto Yordani,^d na mwili wako utaponywa, nawe utaku- wa safi.” **11** Ndipo Naamani akakasirika, akaanza kuondo- ka akisema: “Nilisema moyo- ni mwangu, ‘Atatoka na kuni- jia na kusimama hapa na kuli- ta jina la Yehova Mungu wake, akitikisa mkono wake kwenda mbele na nyuma juu ya uko- ma ili auponye.’ **12** Je, Aba- na na Farpari, mito ya Dama- sko,^e si bora kuliko maji yote ya Israeli? Je, siwezi kuoga humo na kuwa safi?” Ndipo akageuka na kwenda zake kwa hasira kali.

13 Basi watumishi wake wa- kamkaribia na kumwambia: “Baba yangu, kama nabii huyo

SURA YA 5

a Kum 32:39

b 1Fa 17:24
1Fa 19:16
2Fa 3:11, 12
2Fa 8:4c Law 14:7
Hes 19:4

d Yoh 9:6, 7

e Isa 7:8

Safu ya 2

a 2Fa 5:10

b Ayu 33:25

c Lu 4:27
Lu 5:13

d Lu 17:15, 16

e Zb 96:4, 5
Isa 43:10

f Mt 10:8

angekwambia ufanye jambo fulani lisilo la kawaida, je, hungefanya? Je, wakati huu hupaswi kufanya zaidi, kwa kuwa amekuambia tu, ‘Oga, uwe safi?’” **14** Ndipo aka- shuka mtoni na kujitumbuki- za* mara saba katika Mto Yor- dani, kama alivyosema mtu wa Mungu wa kweli.^a Kisha mwili wake ukaponywa ukawa kama mwili wa mvulana mdo- go,^b akawa safi.^c

15 Kisha akarudi kwa yule mtu wa Mungu wa kweli,^d yeye na msafara wake wote,* akasi- mama mbele yake na kusema: “Sasa najua kwamba hakuna Mungu mahali pengine popo- te duniani isipokuwa Israeli.^e Sasa, tafadhali, pokea zawa- di^f kutoka kwangu mimi mtu- mishi wako.” **16** Hata hivyo, Elisha akasema: “Kwa haki- ka kama Yehova anavyoishi ambaye ninamtumikia,* sitai- pokea.”^f Akamsihi sana aipo- kee, lakini akazidi kukataa. **17** Hatimaye Naamani akase- ma: “Ikiwa hutaipokea, tafa- dhali, mimi mtumishi wako ni- naomba udongo wa nchi hii, kiasi kinachoweza kubebwa na nyumbu wawili, kwa saba- bu mimi mtumishi wako sitae- ndelea kutoa dhabihu ya ku- teketezwa wala dhabihu kwa miungu mingine yoyote isi- pokuwa kwa Yehova. **18** La- kini Yehova anisamehe mimi mtumishi wako kwa jambo hili moja: Bwana wangu anapoi- ngia katika nyumba ya* Ri- moni ili kusujudu humo, yeye huegemea mkono wangu, kwa hiyo ninalazimika kusujudu

5:14 *Au “kujizamisha.” **5:15** *Tnn., “kambi yake yote.” ^aTnn., “baraka.” **5:16** *Tnn., “ninasimama mbele zake.” **5:18** *Au “hekalu la.”

katika nyumba ya Rimoni. Nitakapokuwa nikisujudu katika nyumba ya Rimoni, tafadhali, naomba Yehova anisamehe mimi mtumishi wako kwa kufanya jambo hilo.” **19** Basi Elisha akamwambia: “Nenda kwa amani.” Baada ya kuondoka na kusafiri umbali fulani, **20** Gehazi^a mtumishi wa Elisha mtu wa Mungu wa kweli^b akasema moyoni mwake: ‘Tazama, Bwana wangu amemwacha huyu Naamani Msiria^c aende zake kwa kukataa kupokea vitu alivyoleta. Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, nitakimbia na kumfuata, nichukue kitu fulani kutoka kwake.’ **21** Kwa hiyo Gehazi akamfuata mbio Naamani. Naamani alipoona mtu fulani akimfuata mbio, akashuka kutoka kwenye gari lake na kwenda kumpokea, akamuuliza: “Je, mambo yote yako sawa?” **22** Akasema: “Mambo yote yako sawa. Bwana wangu amenituma nikwambie, ‘Tazama! Sasa hivi vijana wawili kutoka kwa wana wa manabii wamekuja kwangu kutoka katika eneo lenye milima la Efraimu. Tafadhali, wape talanta moja ya fedha na mavazi mawili.’”^d **23** Naamani akasema: “Haya, chukua talanta mbili.” Naye akamsihi sana azipokee,^e akafunga talanta mbili za fedha katika mifuko miwili, pamoja na mavazi mawili, akawapa watumishi wake wawili, wakambebea vitu hivyo.

24 Alipofika Ofeli,* akavi-chukua kutoka mikononi mwao, akaviweka nyumbani, na kuwaruhusu watu

5:24 *Eneo fulani kule Samaria, inawezekana ni kilima au ngome.

SURA YA 5

a 2Fa 4:12
2Fa 8:4

b 1Fa 17:24

c 2Fa 5:1
Lu 4:27

d 2Fa 5:5

e 2Fa 5:16

Safu ya 2

a Mdo 5:8,9

b Mt 10:8
Lu 12:15
Mdo 20:33
1Ti 6:10

c 2Fa 5:1

d Kut 4:6
Hes 12:10

SURA YA 6

e 2Fa 2:3, 5
2Fa 9:1

hao waende zao. Walipoondoka, **25** akaingia na kusimama karibu na bwana wake. Sasa Elisha akamuuliza: “Umetoka wapi, Gehazi?” Lakini akajibu: “Mimi mtumishi wako sikwenda mahali popote.”^a **26** Ndipo akamwambia: “Je, moyo wangu haukuwa pamoja nawe wakati yule mtu aliposhuka kutoka kwenye gari lake ili kukupokea? Je, huu ni wakati wa kupokea fedha au kupokea mavazi au mashamba ya mizeituni au mashamba ya mizabibu au kondoo au ng’ombe au watumishi wa kiume au watumishi wa kike?”^b **27** Sasa ukoma wa Naamani^c utashikamana nawe pamoja na wazao wako milele.” Mara moja akaondoka mbele yake akiwa na ukoma, mweupe kama theluji.^d

6 Wana wa manabii^e wakamwambia Elisha: “Tazama! Mahali tunapokaa pamoja nawe ni padogo sana kwetu. **2** Tafadhali, acha twende Yordani. Kila mmoja wetu achukue gogo kutoka sehemu hiyo na kujenga huko mahali tunapoweza ku-kaa.” Akawaambia: “Nendeni.” **3** Mmoja wao akamwambia: “Tafadhali, unaweza kwenda pamoja nasi watumishi wako?” Basi akasema: “Nitakwenda.” **4** Kwa hiyo akaenda pamoja nao, wakafika Yordani na kuanza kukata miti. **5** Mmoja wao alipokuwa akikata mti, shoka likaanguka majini, akasema kwa sauti: “Ole wangu, bwana wangu, liliazimwa!” **6** Mtu wa Mungu wa kweli akauliza: “Limeanguka wapi?” Basi akamwonyesha mahali hapo. Ndipo Elisha akakata kipande cha mti na kukitupa

hapo, akalifanya shoka lielee. **7** Akasema: "Lichukue." Akaunyoosha mkono wake na kulichukua.

8 Sasa mfalme wa Siria alienda kupigana vita na Waisraeli.^a Akashauriana na watumishi wake na kuwaambia: "Nitapiga kambi pamoja nanyi mahali fulani na fulani." **9** Kisha mtu wa Mungu wa kweli^b akamtumia mfalme wa Israeli ujumbe huu: "Jihadhari usipitie mahali hapa, kwa sababu hapa ndipo Wasiria wanaposhukia." **10** Basi mfalme wa Israeli akatuma ujumbe mahali ambapo mtu wa Mungu wa kweli alikuwa amemwonya kupahusu. Mtu wa Mungu wa kweli akaendelea kumwonya, naye mfalme akaepuka mahali hapo mara kadhaa.*^c

11 Jambo hilo likamkasirisha sana mfalme* wa Siria, kwa hiyo akawaita watumishi wake na kuwauliza: "Niambi-ni! Ni nani miongoni mwetu aliye upande wa mfalme wa Israeli?" **12** Kisha mmoja wa watumishi wake akajibu: "Hakuna yeyote miongoni mwetu, bwana wangu mfalme! Nabii Elisha aliye Israeli ndiye humwambia mfalme wa Israeli mambo unayosema katika chumba chako mwenyewe cha kulala."^d **13** Mfalme akasema: "Nendeni mkatafute mahali alipo, ili niwatume watu wamkamate." Baadaye mfalme akaambiwa, "Yuko Dothani."^e **14** Mara moja akapeleka huko farasi na magari ya vita, na pia jeshi kubwa; likaja usiku na kulizunguka jiji hilo.

6:10 *Au "zaidi ya mara moja au mbili."
6:11 *Tnn., "lilikasirisha sana moyo wa mfalme."

SURA YA 6

a 1Fa 20:1, 34
1Fa 22:31

b 1Fa 17:24

c Mt 2:12

d Da 2:22, 28

e Mwa 37:16, 17

Safu ya 2

a Kut 14:13
Zb 3:6

b 2Sa 22:31
2Nya 32:7
Zb 18:2
Zb 27:3
Zb 46:7
Zb 55:18
Zb 118:11
Ro 8:31

c Mdo 7:56

d 2Fa 2:11
Zb 68:17
Zek 6:1

e Zb 34:7
Mt 26:53

f Mwa 19:10, 11

g 1Fa 16:29

15 Mtumishi* wa mtu wa Mungu wa kweli alipoamka asubuhi na mapema na kuto-ka nje, aliona jeshi lenye farasi na magari ya vita yakiwa yamezunguka jiji. Mara moja mtumishi huyo akamwambia: "Ole wetu, bwana wangu! Tutafanya nini?" **16** Lakini Elisha akamwambia: "Usiogope!^a Kwa maana wale walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao."^b **17** Ndi-po Elisha akaanza kusali na kusema: "Ee Yehova, tafadhali, mfungue macho yake, ili aone."^c Mara moja Yehova akamfungua macho mtumishi huyo naye akaona, na tazama! eneo lenye milima lilikuwa limejaa farasi na magari ya vita ya moto^d kumzunguka Elisha pande zote.^e

18 Wasiria waliposhuka kueleka mahali alipokuwa, Elisha akasali kwa Yehova na kusema: "Tafadhali, lipige kwa upofu taifa hili."^f Basi akawapiga kwa upofu kama Elisha alivyooomba. **19** Sasa Elisha akawaambia: "Njia yenyewe si hii, na jiji lenyewe si hili. Nifuatani, nami nitawapeleka kwa mtu mnayemtafuta." Hata hivyo, aliwapeleka Samaria.^g

20 Walipofika Samaria, Elisha akasema: "Ee Yehova, wafungue macho ili waone." Kwa hiyo, Yehova akawafungua macho, nao wakao-na kwamba walikuwa katikati ya Samaria. **21** Mfalme wa Israeli alipowaona, alimuu-liza Elisha, "Je, niwaue, baba yangu, niwaue?" **22** Lakini Elisha akajibu: "Usiwaue. Je, unawaua wale ambao umewachukua mateka kwa upanga

6:15 *Au "Mhudumu."

wako na kwa upinde wako? Wape mikate na maji ili wale na kunywa^a na kurudi kwa bwana wao.” **23** Basi akawaandalia karamu kubwa, nao wakala na kunywa, kisha akawaruhusu warudi kwa bwana wao. Makundi ya wavamizi ya Wasiria^b hayakurudi tena katika nchi ya Israeli.

24 Baadaye Ben-hadadi mfalme wa Siria akalikusanya pamoja jeshi lake lote* na kupanda kwenda kulizingira jiji la Samaria.^c **25** Kwa hiyo kukawa na njaa kali^d sana huko Samaria, nao wakalizingira jiji hilo mpaka kichwa cha punda^e kikawa na thamani ya vipande 80 vya fedha, na robo ya kipimo cha kabi* cha mavi ya njiwa ikawa na thamani ya vipande vitano vya fedha. **26** Mfalme wa Israeli alipokuwa akipita juu ya ukuta, mwanamke fulani akamwambia hivi kwa sauti: “Tusaidie, Ee bwana wangu mfalme!” **27** Mfalme akasema: “Yehova asipokusaidia, nitakupa msaada kutoka wapi? Kutoka kwenye uwanja wa kupuria? Au kutoka katika shinikizo la divai au mafuta?” **28** Mfalme akamuuliza: “Una shida gani?” Akamjibu: “Mwanamke huyu aliniambia, ‘Mtoe mwana wako tumle leo, na mwanangu tutamla kesho.’” **29** Basi tukamchemsha mwanangu na kumla.^g Siku iliyofuata nikamwambia, ‘Mlete mwana wako tumle.’ Lakini akamficha mwanawe.”

30 Mara tu mfalme aliposikia maneno ya mwanamke

6:24 *Tnn., “akaikusanya pamoja kambii yake yote.” **6:25** *Kabi moja ilikuwa sawa na lita 1.22. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 6

a Met 25:21
Ro 12:20

b 2Fa 5:2

c Kum 28:52
1Fa 20:1

d Law 26:26
Kum 28:15, 17

e Kum 14:3
Eze 4:14

f Law 26:29
Kum 28:53-57
Eze 5:10

g Omb 4:10

Safu ya 2

a Mwa 37:29
1Fa 21:27

b Yer 38:4

c 1Fa 18:13
1Fa 21:9, 10

SURA YA 7

d Kum 32:36
2Fa 7:18

huyo, akayararua mavazi yake.^a Alipokuwa akipita juu ya ukuta, watu wakaona kwamba alikuwa amevaa nguo za magunia ndani ya nguo zake. **31** Mfalme akasema: “Mungu na aniadhibu, tena vikali, ikiwa Elisha mwana wa Shafati hatakatwa kichwa leo!”^b

32 Elisha alikuwa ameketi nyumbani kwake pamoja na wazee. Mfalme akamtuma mtu amtangulie, lakini kabla ya mjumbe huyo kufika, Elisha akawaambia wazee hao: “Je, mmeona jinsi ambavyo mwana huyu wa muuaji^c amemtuma mtu aje kunikata kichwa? Mjumbe huyo atakapofika, fungeni mlango, nanyi muusukume ili asiingie. Je, bwana wake hayuko nyuma yake aki-mfuata?” **33** Alipokuwa akizungumza nao, mjumbe huyo akaja kwake, mfalme akasema: “Msiba huu unatoka kwa Yehova. Kwa nini niendeleo kumngojea Yehova?”

7 Sasa Elisha akasema: “Sikiliza neno la Yehova. Yehova anasema hivi: ‘Kesho karibu wakati kama huu sea moja* ya unga laini itakuwa na thamani ya shekeli moja, na sea mbili za shayiri zitakuwa na thamani ya shekeli moja[#] katika lango la[^] Samaria.’”^d **2** Ndipo kama nda msaidizi ambaye mfalme alimtegemea akamwambia hivi mtu wa Mungu wa kweli: “Hata Yehova akiyafungua malango ya mbinguni ya mafuriko, je, kweli jambo hilo

7:1 *Sea moja ilikuwa sawa na lita 7.33 (vibaba 6.66). Angalia Nyongeza B14. [#]Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. [^]Au “masoko ya.”

linaweza kutokea?”*^a Ndipo Elisha akamwambia, “Utaona kwa macho yako mwenyewe,^b lakini hutakula vyakula hivyo.”^c

3 Kulikuwa na watu wanne wenye ukoma kwenye lango la jiji,^d nao wakaambiana: “Kwa nini tuketi hapa mpaka tufe?”

4 Tukisema, ‘Acheni tuingie jijini,’ na bado kuna njaa kali jijini,^e tutafia humo. Nasi tukiketi hapa, bado tutakufa. Basi sasa twende zetu kwenye kambi ya Wasiria. Wakituruhusu tuishi, tutaishi; lakini wakituuu, basi tutakufa.” **5** Kwa hiyo wakaondoka jioni giza lilipoanza kuingia, wakaingia kwenye kambi ya Wasiria. Walipofika kandokando ya kambi ya Wasiria, hakukuwa na mtu yeyote.

6 Kwa maana Yehova alikuwa amesababisha kambi ya Wasiria isikie sauti ya magari ya vita na farasi, sauti ya jeshi kubwa.^f Basi wakaambiana: “Tazama! Mfalme wa Israeli amekodi wafalme wa Wahiti na wafalme wa Misri watushambulie!” **7** Mara moja wakaondoka na kukimbia katika giza la jioni, wakaacha mahema yao, farasi wao, punda wao, na kambi yote kama ilivyokuwa, wakakimbia ili kuochoa maisha yao.*

8 Watu hao wenye ukoma walipokaribia kambi hiyo, wakaingia ndani ya hema moja na kuanza kula na kunywa. Wakachukua fedha, dhahabu, na mavazi kutoka humo, wakaenda na kuficha vitu hivyo. Kisha wakarudi na kuingia katika hema lingine, wakachu-

7:2 * Tnn., “kweli neno hilo linaweza kutimia?” 7:7 * Au “nafsi zao.”

SURA YA 7

a Hes 14:11

b Hes 11:23

c 2Fa 7:17

d Law 13:45, 46

e 2Fa 6:25

f Kum 28:7
2Sa 5:24

Safu ya 2

a 2Fa 6:25
2Fa 6:28, 29

b Yos 8:4, 12
Amu 20:29, 37

kua vitu kutoka humo na kwe-nda kuvificha.

9 Mwishowe wakaambiana: “Jambo tunalofanya si sawa. Leo ni siku ya habari njema! Tukisitasita na kusubiri mpa-ka mapambazuko, tutastahili kuadhibiwa. Twendeni sasa tukaiambie nyumba ya mfalme habari hizi.” **10** Basi wakaenda na kuwaita kwa sauti walinzi wa malango ya jiji na kuwaambia: “Tulienda kwenye kambi ya Wasiria, lakini hakukuwa na mtu yeyote huko—hatukusikia sauti ya yeyote. Kulikuwa tu na farasi na punda waliofungwa na mahema yaliyoachwa kama yalivyokuwa.” **11** Mara moja walinzi hao wa malango wakatanga-za habari hizo, nazo zikafika nyumbani kwa mfalme.

12 Mara moja mfalme akaamka usiku na kuwaambia watumishi wake: “Acheni niwaambie yale ambayo Wasiria wametutendea. Wanajua kwamba tuna njaa,^a kwa hiyo walitoka kambini na kujificha shambani, wakisema, ‘Watatoka jijini, nasi tutawakamata wakiwa hai na kuingia jijini.’”^b

13 Ndipo mmoja wa watumishi wake akasema: “Tafadhali, waruhusu baadhi ya wanaume wachukue farasi watano kati ya wale waliobaki jijini. Hali itakayowapata itakuwa sawa na hali itakayoupata umati wa Waisraeli unaobaki hapa. Hali yao itakuwa sawa na ya umati wa Waisraeli ambao waliangamia. Basi na tuwatume waende tuone hali itakavyokuwa.” **14** Wakachukua magari mawili pamoja na farasi, na mfalme akawatuma kwenye kambi ya Wasiria na kuwaambia: “Nendeni mwone

hali ilivyo.” **15** Wakawafuata mpaka Yordani, na mavazi na vyombo ambavyo Wasiria walikuwa wametupa walipokuwa wakikimbia kwa hofu vilikuwa vimetapakaa njia yote. Kisha wajumbe hao wakarudi na kumletea mfalme habari.

16 Ndipo watu wakatoka na kuipora kambi ya Wasiria, hivi kwamba sea moja ya unga laini ikawa na thamani ya shekeli moja, na sea mbili ya shayiri ikawa na thamani ya shekeli moja, kulingana na neno la Yehova.^a **17** Mfalme alimweka yule kamanda msaidizi awe msimamizi wa lango, kamanda ambaye mfalme alimtegemea, lakini watu wakamkanyagakanyaga langoni hadi akafa, kama yule mtu wa Mungu wa kweli alivyokuwa amemwambia mfalme alipokwenda kumwona. **18** Ilitendeka kama mtu wa Mungu wa kweli alivyokuwa amemwambia mfalme: “Kesho wakati kama huu, sea mbili za shayiri zitakuwa na thamani ya shekeli moja, na sea moja ya unga laini itakuwa na thamani ya shekeli moja katika lango la Samaria.”^b **19** Lakini yule kamanda msaidizi alikuwa amemwambia mtu wa Mungu wa kweli: “Hata Yehova akiyafungua malango ya mbinguni ya mafuriko, je, kweli jambo hilo linaweza kutokea?”* Elisha akamjibu: “Utaona kwa macho yako mwenyewe, lakini hutakula vyakula hivyo.” **20** Hivyo ndivyo ilivyotokea kwake, kwa maana watu walimkanyaga-kanyaga langoni hadi akafa.

7:19 * Tnn., “kweli neno hilo linaweza kutimia?”

SURA YA 7

a Hes 23:19
2Fa 7:1
Isa 55:10, 11

b 2Fa 7:1, 2

Safu ya 2

SURA YA 8

a 2Fa 4:32-35

b Law 26:19
Kum 28:15, 23
1Fa 17:1

c Yos 13:2, 3

d 2Fa 2:14
2Fa 2:20, 21
2Fa 3:17
2Fa 4:4, 7
2Fa 6:5-7
2Fa 7:1

e 2Fa 4:32-35

f Hes 36:9

8 Elisha alimwambia hivi yule mwanamke ambaye alikuwa amemfufua mwana-we:^a “Ondoka uende, wewe pamoja na familia yako, uishi kama mgeni mahali popote unapoweza kuishi, kwa maana Yehova ametangaza kwamba kutakuwa na njaa kali^b nchini kwa miaka saba.” **2** Basi yule mwanamke akaondoka na kufanya kama mtu wa Mungu wa kweli alivyomwambia. Akaenda pamoja na familia yake kuishi katika nchi ya Wafilisti^c kwa miaka saba.

3 Baada ya miaka saba, mwanamke huyo akarudi kutoka katika nchi ya Wafilisti, akaenda kumsihi mfalme ili arudishiwe nyumba yake na shamba lake. **4** Sasa mfalme alikuwa akizungumza na Gehazi mtumishi wa yule mtu wa Mungu wa kweli, akamwambia: “Tafadhali, nisimulie mambo yote makuu ambayo Elisha amefanya.”^d **5** Alipokuwa akimsimulia mfalme jinsi Elisha alivyomfufua mto-to aliyekufa,^e yule mwanamke ambaye mwana wake alikuwa amefufuliwa akaja kwa mfalme akimsihi arudishiwe nyumba yake na shamba lake.^f Mara moja Gehazi akasema: “Bwana wangu mfalme, huyu ndiye yule mwanamke, na huyu ndiye mwana wake ambaye Elisha alimfufua.” **6** Ndipo mfalme aka muuliza mwanamke huyo, naye akamsimulia kisa choote. Kisha mfalme akamkabidhi mwanamke huyo kwa ofisa wa makao ya mfalme, akamwambia hivi ofisa huyo: “Rudisha mali yote ya mwanamke huyo na mazao yote ya

shamba lake tangu siku alipotoka nchini hadi sasa.”

7 Elisha alienda Damasko^a wakati Ben-hadadi^b mfalme wa Siria alipokuwa mgonjwa. Ben-hadadi akaambiwa hivi: “Yule mtu wa Mungu wa kweli^c amekuja.” **8** Ndipo mfalme akamwambia Hazaeli:^d “Chukua zawadi, ukakutane na mtu wa Mungu wa kweli.^e Muulize Yehova kupitia kwake, ‘Je, nitapona ugonjwa huu?’” **9** Hazaeli akachukua zawadi na kwenda kukutana naye, alichukua vitu vizuri vya kila aina kutoka Damasko, mizigo iliyoweza kubebwa na ngamia 40. Akaja na kusimama mbele yake na kumwambia: “Mwana wako, Ben-hadadi, mfalme wa Siria amenituma kwako ni kuulize, ‘Je, nitapona ugonjwa huu?’” **10** Elisha akamjibu: “Nenda ukamwambie, ‘Hakika utapona,’ lakini Yehova amenionyesha kwamba hakika atakufa.”^f **11** Elisha akamkazia macho sana Hazaeli mpaka akaona aibu. Kisha yule mtu wa Mungu wa kweli akaanza kulia. **12** Hazaeli akamuuliza: “Bwana wangu, kwa nini unalia?” Akamjibu: “Kwa sababu ninajua madhara utakayowatendea Waisraeli.^g Utakeiteza ngome zao, utawaua kwa upanga wanaume wao mashujaa, utawapondaponda watoto wao, na kuwapasua tumbo wanawake wao wenye mimba.”^h **13** Hazaeli akasema: “Mimi mtumishi wako, ambaye ni mbwa tu, ninawezaje kufanya jambo kama hilo?” Lakini Elisha akasema: “Yehova amenionyesha kwamba wewe utakuwa mfalme wa Siria.”ⁱ

14 Kisha Hazaeli akamwacha Elisha na kurudi kwa

SURA YA 8

a Isa 7:8

b 1Fa 20:1
2Fa 6:24

c 1Fa 17:24

d 1Fa 19:15

e 1Sa 9:8
1Fa 14:2, 3

f 2Fa 8:15

g 2Fa 10:32
2Fa 12:17
2Fa 13:3
Amo 1:3h Kum 28:63
Amo 1:13

i 1Fa 19:15

Safu ya 2

a 2Fa 8:10

b 1Fa 16:8, 10
2Fa 11:1
2Fa 15:8, 10

c 1Fa 19:15

d 2Fa 1:17

e 1Fa 22:50
2Nya 21:3, 5

f 1Fa 12:28-30

g 1Fa 16:32, 33
1Fa 21:25h 2Fa 8:26, 27
2Nya 18:1

i 2Nya 21:6, 7

j Mwa 49:10
2Sa 7:16, 17k 1Fa 11:36
Zb 132:17l Mwa 27:40
2Sa 8:14m 1Fa 22:47
2Nya 21:8-10n Yos 21:13
2Fa 19:8

wana wake, Ben-hadadi akamuuliza: “Elisha alikwambia nini?” Akamjibu: “Alinambia kwamba hakika utapona.”^a **15** Lakini siku iliyofuata, Hazaeli akachukua tandiko, akalitumbukiza ndani ya maji, na kumfunika nalo usoni mpaka akafa.^b Kisha Hazaeli akawa mfalme baada yake.^c

16 Katika mwaka wa tano wa utawala wa Yehoram^d mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli, Yehoshafati alipokuwa mfalme wa Yuda, Yehoram^e mwana wa Mfalme Yehoshafati wa Yuda akawa mfalme. **17** Alikuwa na umri wa miaka 32 alipoanza kutawala, naye alitawala huko Yerusalemu kwa miaka minane. **18** Alitembea katika njia ya wafalme wa Israeli,^f kama walivyofanya watu wa nyumba ya Ahabu,^g kwa maana alikuwa amemwoa binti ya Ahabu,^h naye aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova.ⁱ **19** Lakini Yehova hakutaka kuangamiza Yuda kwa sababu ya Daudi mtumishi wake,^j kwa maana alikuwa amemwahidi atampa yeye na wanawe ta sikuzote.^k

20 Katika siku za Yehoram, Waedomu waliasi dhidi ya Yuda,^l nao wakajichagulia mfalme wao wenyewe.^m **21** Basi Yehoram akavuka kwenda Sairi na magari yake yote ya vita, akaondoka usiku na kuwashinda Waedomu waliokuwa wamemzingira yeye na makamanda wa magari ya vita; na wanajeshi wakakimbilia katika mahema yao. **22** Lakini tangu siku hiyo Waedomu wameendelea kuia-si nchi ya Yuda. Watu wa Libnaⁿ waliasi pia wakati huo.

23 Na mambo mengine katika historia ya Yehoram, mambo yote aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **24** Kisha Yehoram akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.^a Na Ahazia^b mwana wake akawa mfalme baada yake.

25 Katika mwaka wa 12 wa utawala wa Yehoram mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli, Ahazia mwana wa Mfalme Yehoram wa Yuda akawa mfalme.^c **26** Ahazia alikuwa na umri wa miaka 22 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa mwaka mmoja huko Yerusalemu. Mama yake alitwa Athalia,^d mjukuu wa* Mfalme Omri^e wa Israeli. **27** Alite-mbea katika njia ya nyumba ya Ahabu^f na kuendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, kama nyumba ya Ahabu, kwa maana alikuwa ameo kutoka katika nyumba ya Ahabu.^g **28** Basi Ahazia alienda pamoja na Yehoram mwana wa Ahabu kupigana vita na Mfalme Hazaeli wa Siria kule Ramothi-gileadi,^h lakini Wasiria wakamjeruhi Yehoram.ⁱ **29** Kwa hiyo Mfalme Yehoram akarudi Yezreeli^j ili apone majeraha aliyopata kutoka kwa Wasiria huko Rama alipopigana na Mfalme Hazaeli wa Siria.^k Ahazia mwana wa Yehoram mfalme wa Yuda akashuka kwenda Yezreeli kumwona Yehoram mwana wa Ahabu, kwa saba alikuwa amejeruhiwa.*

8:26 *Tnn., "binti ya." 8:29 *Au "mgonjwa."

SURA YA 8

a 1Fa 2:10
2Nya 21:18-20

b 1Nya 3:10, 11
2Nya 21:16, 17
2Nya 22:1, 2

c 2Fa 9:29

d 2Fa 11:1
2Fa 11:13, 16

e 1Fa 16:16, 23

f 1Fa 16:33

g 2Fa 8:16, 18
2Nya 22:3, 4

h Yos 21:38
1Fa 22:2, 3

i 1Fa 19:17
2Nya 22:5

j Yos 19:17, 18
1Fa 21:1
2Nya 22:6

k 2Fa 9:15

Safu ya 2

SURA YA 9

a 2Fa 8:25, 28

b 1Fa 19:16, 17

c 2Nya 22:7

d 1Fa 19:16

e 1Fa 18:4
1Fa 19:2
1Fa 21:15, 25
Lu 18:7

9 Kisha nabii Elisha akamwita mmoja wa wana wa manabii na kumwambia: "Jifunge mavazi yako kiunoni, na uchukue haraka chupa hii ya mafuta uende Ramothi-gileadi.^a **2** Utakapofika huko, mtafute Yehu^b mwana wa Yehoshafati mwana wa Nimshi; ingia ndani, umchukue kutoka miongoni mwa ndugu zake, na kumpeleka katika chumba cha ndani zaidi. **3** Kisha chukua chupa ya mafuta, uyamimine juu ya kichwa chake na kusema, 'Yehova anasema hivi: "Ninakutia mafuta uwe mfalme wa Israeli."^c Halafu ufungue mlango na kukimbia bila kukawia."

4 Basi yule mtumishi wa nabii akaenda Ramothi-gileadi. **5** Alipofika, aliwakuta wakuu wa majeshi wakiwa wameketi pamoja. Akasema: "Nina ujumbe wako, ewe mkuu." Yehu akamuuliza: "Ni ujumbe wa nani kati yetu?" Akasema: "Ujumbe wako, ewe mkuu." **6** Basi Yehu akainuka na kuingia ndani ya nyumba; mtumishi huyo akamiminia yale mafuta juu ya kichwa na kumwambia, "Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: 'Ninakutia mafuta uwe mfalme wa watu wa Yehova, uwe mfalme wa Israeli.'^d **7** Unapaswa kuiangamiza nyumba ya Ahabu bwana wako, nami nitailipizia kisasi damu ya watumishi wangu manabii na watumishi wote wa Yehova ambao Yezebeli aliwaua.^e **8** Na nyumba yote ya Ahabu itaangamiza; nami nitamwangamiza kila mwanamume* wa Ahabu,

9:7 *Tnn., "waliofia mikononi mwa Yezebeli." 9:8 *Tnn., "mtu yeyote anayekojoa ukutani." Huu ni msemu wa Kiebrania wa kuwadharau wanaume.

kutia ndani wasio na uwezo na walio dhaifu katika Israeli.^a **9** Nami nitaifanya nyumba ya Ahabu kuwa kama nyumba ya Yeroboamu^b mwana wa Nebati na kama nyumba ya Baasha^c mwana wa Ahiya. **10** Kuhusu Yezebeli, mbwa watamla katika shamba kule Yezreeli,^d na hakuna yeyote atakayemzika.” Kisha mtumishi huyo akafungua mlango na kukimbia.^e

11 Yehu aliporudi kwa watumishi wa bwana wake, wakamuuliza: “Je, mambo yote yako sawa? Kwa nini mwenda-wazimu huyu alikuja kwako?” Akawajibu: “Ninyi mnajua huyu ni mtu wa aina gani na mambo anayosema.” **12** Lakini wakasema: “Hilo si kweli! Tafadhali tuambia.” Ndiipo akasema: “Aliniambia hivi, halafu akasema, ‘Yehova anasema hivi: “Ninakutia mafuta uwe mfalme wa Israeli.””^f

13 Ndipo kila mmoja wao akavua vazi lake haraka na kulitandika chini ya Yehu kwenye ngazi zilizo wazi,^g nao wakapiga pembe na kusema: “Yehu amekuwa mfalme!”^h **14** Kisha Yehuⁱ mwana wa Yehoshafati mwana wa Nimshi akapanaga njama dhidi ya Yehoramumu.

Yehoramumu alikuwa akilinda huko Ramothi-gileadi,^j yeye na Waisraeli wote, kwa sababu ya Mfalme Hazaeli^k wa Siria. **15** Baadaye Mfalme Yehoramumu akarudi Yezreeli^l ili kuuguzwa majeraha aliyokuwa amepata kutoka kwa Wasiria alipopigana na Mfalme Hazaeli wa Siria.^m

Sasa Yehu akasema: “Mki-kubaliana nami, msimwache yeyote atoroke kutoka jijini na kupeleka habari hii Yez-

SURA YA 9

a 1Fa 21:20, 21

b 1Fa 15:28, 29

c 1Fa 16:11, 12

d 1Fa 21:23

e 2Fa 9:3

f 2Fa 9:6

g Mt 21:7

h 2Sa 15:10
1Fa 1:34, 39

i 1Fa 19:16

j 2Fa 8:28

k 1Fa 19:15
2Fa 8:15
2Fa 10:32l Yos 19:17, 18
1Fa 21:1

m 2Nya 22:6

Safu ya 2

a 2Fa 8:25
2Fa 8:29
2Nya 22:7

reeli.” **16** Kisha Yehu akapanda gari lake na kwenda Yezreeli, kwa maana Yehoramumu alikuwa amelala huko akiwa amejeruhiwa, na Mfalme Ahazia wa Yuda alikuwa ameshuka kwenda kumwona Yehoramumu. **17** Mlinzi aliyekuwa amesimama juu ya mnara huko Yezreeli aliona kundi kubwa la wanaume wa Yehu likija. Mara moja akasema: “Ninaona kundi kubwa la wanaume.” Yehoramumu akasema: “Chukua mpanda farasi mmoja umtume akutane nao, awaulize, ‘Je, mmekuja kwa amani?’” **18** Basi mpanda farasi akaenda kukutana naye, akasema: “Mfalme anauliza, ‘Je, mmekuja kwa amani?’” Lakini Yehu akasema: “Kwa nini unauliza kuhusu ‘amani’? Nifuate!”

Basi yule mlinzi akasema: “Mjumbe aliwafikia, lakini hajarudi.” **19** Kwa hiyo akatuma mpanda farasi wa pili, akawaambia hivi alipowafikia: “Mfalme anauliza hivi: ‘Je, mmekuja kwa amani?’” Lakini Yehu akasema: “Kwa nini unauliza kuhusu ‘amani’? Nifuate!”

20 Basi yule mlinzi akasema: “Aliwafikia, lakini hajarudi, na uendeshaji wa gari ni kama wa Yehu mjukuu* wa Nimshi, kwa maana yeye huendesha gari kama mwendawazimu.” **21** Yehoramumu akasema: “Fungeni farasi kwenye gari!” Basi farasi wakafungwa kwenye gari lake la vita, na Yehoramumu mfalme wa Israeli na Ahazia^a mfalme wa Yuda wakaondoka kila mmoja kwenye gari lake la vita ili ku-

9:20 *Tnn., “mwana.”

kutana na Yehu. Wakakutana naye katika shamba la Nabothi,^a Myezreeli.

22 Mara tu Yehoramu alipomwona Yehu, akamuuliza: "Yehu, umekuja kwa amani?" Lakini akamjibu: "Kunaweza je kuwa na amani wakati kuna ukahaba wa Yezebeli^b mama yako na ulozi wake mwingi?"^c **23** Mara moja Yehoramu akageuzi gari lake ili akimbie, akamwambia Ahazia: "Tumedanganywa, Ahazia!"

24 Yehu akachukua upinde wake na kumpiga mshale Yehoramu katikati ya mabega, na mshale huo ukatokea moyoni mwake, naye akaanguka ndani ya gari lake la vita. **25** Kisha akamwambia Bidkari kamanda wake msaidizi: "Mwinue na umtupe katika shamba la Nabothi, Myezreeli.^d Kumbuka kwamba mimi na wewe tulipokuwa tukiendesha magari ya farasi* tukimfuata Ahabu baba yake, Yehova mwenyewe alitangaza hivi dhidi yake:"^e **26** "Kwa hakika kama nilivyoona damu ya Nabothi^f na damu ya wanawake jana," asema Yehova, "nitakulipa^g wewe katika shamba hilihili," asema Yehova.^h Basi sasa mwinue na umtupe katika shamba hili, kulingana na neno la Yehova."^h

27 Mfalme Ahazia wa Yuda alipoona hayo, alikimbia kupitia njia ya nyumba ya bustani. (Baadaye Yehu akamfuatia na kusema: "Muueni yeye pia!" Kwa hiyo wakampiga ndani ya gari akipanda kuelekea Guri, karibu na mji wa Ibleamu.) Lakini akaendelea kukimbia mpaka Megido, akafia huko.

9:25 *Tnn., "makundi ya magari ya farasi."

SURA YA 9

a 1Fa 21:1, 15

b 1Fa 16:31
1Fa 18:4
1Fa 19:2
1Fa 21:7c Law 20:6
Kum 18:10
1Fa 18:19

d 1Fa 21:19

e 1Fa 21:29

f Mwa 4:8, 10
Zb 9:12
Zb 72:14g Mwa 9:5
Law 24:17

h 1Fa 21:24

i 2Fa 8:29
2Nya 22:7

j Yos 17:11

Safu ya 2

a 2Sa 5:7

b 2Fa 8:24
2Nya 22:2

c 1Fa 21:1

d 1Fa 16:31
1Fa 21:25

e 1Fa 16:15-19

f Kut 32:26
Zb 94:16

g 1Fa 16:31

h 2Fa 9:10

i Isa 55:10, 11

j 1Fa 21:23

28 Kisha watumishi wake wakambeba ndani ya gari mpaka Yerusalemu, wakamzika katika kaburi lake pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.^a

29 Mfalme Ahazia alianza kutawala Yuda katika mwaka wa 11 wa utawala wa Yehoramu mwana wa Ahabu.)^b

30 Yehu alipofika Yezreeli,^c Yezebeli^d akasikia habari hizo. Basi akapaka macho yake wanja na kupamba nywele zake, akatazama chini kupitia dirishani. **31** Yehu alipokuwa akiingia langoni, Yezebeli akasema: "Je, mambo yalimwenda sawa Zimri, aliyemua bwana wake?"^e **32** Yehu akatazama juu dirishani na kuuliza: "Ni nani aliye upande wangu? Ni nani?"^f Mara moja maofisa wawili au watatu wa makao ya mfalme wakamtazama wakiwa dirishani. **33** Yehu akasema: "Mtupeni chini mwanamke huyo!" Kwa hiyo wakamtupa chini, na kiasi fulani cha damu yake kikata-pakaa kwenye ukuta na farasi, kisha Yehu akamkanyaganyaga. **34** Baada ya hayo akaingia ndani, akala na kunywa. Halafu akasema: "Tafadhali, mchukueni mwanamke huyu aliyelaaniwa mkamzike. Kwa maana yeye ni binti ya mfalme."^g **35** Lakini walipoenda kumzika, hawakupata chochote isipokuwa fuvu la kichwa na miguu na viganja vya mikono.^h **36** Waliporudi na kumwambia Yehu, akasema: "Jambo hilo linatimiza neno hili la Yehovaⁱ alilosema kupitia mtumishi wake Eliya, Mtishbi: 'Katika shamba la Yezreeli, mbwa wataula mwili wa Yezebeli.'^j

37 Na maiti ya Yezebeli itakuwa kama mbolea katika shamba la Yezreeli, ili watu wasiseme: "Huyu ni Yezebeli.""

10 Sasa Ahabu^a alikuwa na wana 70 kule Samaria. Kwa hiyo Yehu akaandika barua, akazituma Samaria kwa wakuu wa Yezreeli, wazee,^b na walezi wa watoto wa Ahabu,^{*} akisema: **2** "Sasa barua hii itakapowafikia ninyi, wana wa bwana wenu watakuwa pamoja nanyi, na pia mtakuwa na magari ya vita, farasi, jiji lenye ngome, na silaha. **3** Chagueni mwana bora na anayefaa^{*} kabisa kati ya wana wa bwana wenu na mumweke kwenye kiti cha ufalme cha baba yake. Kisha mpigane vita kwa ajili ya nyumba ya bwana wenu."

4 Lakini wakaogopa sana na kusema: "Tazama! Ikiwa ufalme wawili hawakuweza kupigana naye,^c sisi tutawezaje kupigana naye?" **5** Basi msimamizi wa jumba la mfalme,^{*} gavana wa jiji, wazee, na wale walezi wakamtumia Yehu ujumbe huu: "Sisi ni watumishi wako, nasi tutafanya mambo yote utakayotuongia. Hatutamweka yeyote kuwa mfalme. Fanya jambo lolote unaloona ni jema machoni pako."

6 Ndipo Yehu akawaandikia barua ya pili, akisema: "Ikiwa mko upande wangu na mko tayari kunitii, leteni vichwa vya wana wa bwana wenu na mje kwangu kesho wakati kama huu kule Yezreeli."

Wana 70 wa mfalme walikuwa pamoja na wanaume mashuhuri wa jiji waliokuwa

10:1 *Tnn., "walezi wa Ahabu." 10:3 *Au "mnyoofu." 10:5 *Tnn., "nyumba."

SURA YA 10

a 1Fa 16:29

b 1Fa 21:8

c 2Fa 9:24, 27

Safu ya 2

a 1Fa 21:21

b 2Fa 9:14, 24

c 1Sa 15:29
Isa 14:27

d 1Fa 21:19-24
2Fa 9:7, 36

e 1Fa 18:19
2Fa 23:19, 20

f 1Fa 21:21

g 2Fa 8:29
2Fa 9:21, 27
2Nya 22:1

wakiwalea. **7** Mara tu barua hiyo ilipowafikia, wakawachukua wana wa mfalme, wanau-me 70,^a na kuwachinja, kisha wakaweka vichwa vyao ndani ya vikapu, wakampelekea kule Yezreeli. **8** Mjumbe akaenda kwa Yehu na kumwambia: "Wameleta vichwa vya wana wa mfalme." Kwa hiyo akasema: "Viwekeni katika marundo mawili kwenye lango la jiji mpaka asubuhi." **9** Yehu alipotoka asubuhi, alisimama mbele ya watu wote na kuwambia: "Ninyi hamna hatia.^{*} Naam, nilipanga njama dhidi ya bwana wangu, nikamuua,^b lakini ni nani aliyewaua hawa wote? **10** Basi jueni kwamba hakuna neno hata moja la Yehova ambalo Yehova amesema dhidi ya nyumba ya Ahabu litakalokosa kutimia,^c na Yehova amefanya yale aliyosema kupitia mtumishi wake Eliya."^d **11** Basi Yehu akawaua watu wote waliobaki wa nyumba ya Ahabu kule Yezreeli, na pia watu wake wote mashuhuri, marafiki zake, na makuhani wake,^e hakumwacha mtu yeyote wa nyumba yake akiwa hai.^f

12 Kisha akaondoka na kuelekea Samaria. Njiani kulikuwa na nyumba ya kuwakatia kondoo manyoya. **13** Huko Yehu akakutana na ndugu za Mfalme Ahazia^g wa Yuda, naye akawauliza, "Ninyi ni nani?" Wakasema: "Sisi ni ndugu za Ahazia, nasi tunashuka kwenda kuwajulia hali wana wa mfalme na wana wa mama malkia." **14** Mara moja akasema: "Wakamateni

10:9 *Au "Ninyi ni waadilifu." 10:10 *Tnn., "litakaloanguka ardhini."

wakiwa hai!” Basi wakawakamata wanaume 42 wakiwa hai na kuwachinja kando ya tangi la maji la nyumba ya kuwakatia kondoo manyoya. Haku-mwacha yeyote kati yao aki-wa hai.^a

15 Alipokuwa akiondoka mahali hapo, alikutana na Yehonadabu^b mwana wa Reka-bu^c akija kumpokea. Yehu akamsalimia* na kumuuliza: “Je, moyo wako ni kamili^d kuniele-kea, kama moyo wangu ulivyo kamili kukuelekea?”

Yehonadabu akajibu: “Ndiyo.”

“Ikiwa ndivyo, nipe mkono wako.”

Kwa hiyo akampa mkono wake, na Yehu akamvuta na kum-pandisha kwenye gari lake. **16** Kisha akasema: “Twende pamoja, uone kwamba sivumilii ushindani wowote kumwele-kea* Yehova.”^d Basi wakae-nda pamoja naye katika gari lake la vita. **17** Kisha Yehu akafika Samaria na kuwaua watu wote waliobaki wa nyumba ya Ahabu huko Samaria mpaka alipowaangami-za wote,^e kulingana na neno la Yehova alilomwambia Eliya.^f

18 Tena Yehu akawakusa-nya watu wote na kuwaambia: “Ahabu alimwabudu Baali kwa kiwango kidogo tu,^g lakini Yehu atamwabudu kwa kiwan-go kikubwa zaidi. **19** Basi wakusanyeni manabii wote wa Baali,^h waabudu wake wote, na makuhani wake woteⁱ waje kwangu. Hakikisheni kwa-mba hakuna hata mmoja ata-kayekosa kufika, kwa sababu

10:15 *Au “akambariki.” #Tnn., “mnyoofu.” **10:16** *Au “uone bidii ya-angu kwa ajili ya.”

SURA YA 10

a 2Nya 22:8

b Yer 35:6, 19

c 1Nya 2:55

d Hes 25:11
1Fa 19:10

e 2Fa 9:8
2Nya 22:7

f 1Fa 21:20, 21
2Fa 9:26

g 1Fa 16:32, 33
1Fa 18:22

h 2Fa 3:13

i 2Fa 10:11

Safu ya 2

a 1Fa 16:30, 32

b 2Fa 10:15
Yer 35:6, 19

nina dhabihu kubwa kwa ajili ya Baali. Yeyote atakayekosa kufika hataishi.” Lakini Yehu alikuwa akitenda kwa ujanja ili awaangamize waabudu wa Baali.

20 Yehu akaendelea kuse-ma: “Tangazeni* kusanyiko takatifu kwa ajili ya Baali.” Basi wakalitangaza. **21** Ki-sha Yehu akatuma ujumbe ko-tekote katika Israeli, na waabudu wote wa Baali waka-ja. Hakuna hata mmoja wao ambaye hakuja. Wakaingia katika nyumba ya* Baali,^a na nyumba ya Baali ikajaa kuto-ka mwisho mmoja hadi mwisho mwingine. **22** Akamwa-mbia msimamizi wa chumba cha mavazi: “Leta mavazi kwa ajili ya waabudu wote wa Baa-li.” Basi akawaleta mavazi. **23** Halafu Yehu na Yehonada-bu^b mwana wa Rekabu wakai-ngia katika nyumba ya Baa-li. Yehu akawaambia waabu-du wa Baali: “Tafuteni kwa uangalifu mhakikishe kwa-mba hakuna mwabudu yeyo-te wa Yehova humu ndani isi-pokuwa waabudu wa Baali.” **24** Mwishowe wakaingia nda-ni ili kutoa dhabihu mbali-mbali na dhabihu za kuteke-tezwa. Yehu alikuwa ameweka wanaume wake 80 nje na ku-waambia, “Yeyote kati ya wa-naume ninaowatia mikononi mwenu akiponyoka, mtalipia uhai wake kwa uhai wenu.”*

25 Mara tu alipomaliza ku-toa dhabihu ya kuteketezwa, Yehu akawaambia hivi wali-nzi* na makamanda wasaidizi:

10:20 *Tnn., “Takaseni.” **10:21** *Au “hekalu la.” **10:24** *Au “mtalipia nafsi yake kwa nafsi yenu.” **10:25** *Tnn., “wakimbajia.”

“Ingieni ndani na kuwaua! Msimwache yeyote aponyoke!”^a Basi walinzi na makamanda wasaidizi wakawaua kwa upanga na kuwatupa nje, wa-kaingia mpaka kwenye chumba kitakatifu cha ndani cha* nyumba hiyo ya Baali. **26** Kisha wakatoa nje nguzo takatifu^b za nyumba ya Baali na kuiteketeza kila nguzo.^c **27** Wakabomoa nguzo takatifu^d ya Baali na kuibomoa nyumba ya Baali,^e na kuigeuza kuwa vyoo, na hivyo ndivyo ilivyo mpaka leo.

28 Kwa hiyo Yehu akakomeshisha kabisa ibada ya Baali katika Israeli. **29** Hata hivyo, Yehu hakugeuka na kuacha dhambi ambazo Yero-boamu mwana wa Nebati alisababisha Waisraeli kute-nda kuhusiana na wale ndama wa dhahabu waliokuwa Betheli na Dani.^f **30** Basi Yehova akamwambia Yehu: “Kwa kuwa umetenda vema na ume-fanya yaliyo sawa machoni pa-angu kwa kutenda mambo yote yaliyokuwa moyoni mwangu niliyokusudia kuitendea nyumba ya Ahabu,^g vizazi vinne vya wana wako vitaketi kwe-nye kiti cha ufalme cha Israe-li.”^h **31** Lakini Yehu hakuwa mwangalifu kutembea katika Sheria ya Yehova Mungu wa Israeli kwa moyo wake wote.ⁱ Hakugeuka na kuacha dhambi ambazo Yero-boamu alisababi-sha Waisraeli kutenda.^j

32 Siku hizo Yehova alianza kupunguza* eneo la Israeli, eneo moja baada ya lingine. Hazaeli akaendelea kuwasha-

10:25 *Tnn., “kwenye jiji la,” labda ni jengo lililokuwa kama ngome. 10:32 *Tnn., “kukata.”

SURA YA 10

a Kut 32:26, 27
Kum 13:6-9
Eze 9:5

b Law 26:1

c Kum 7:25

d Law 26:30
Kum 7:5

e 1Fa 16:30, 32

f 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33
Ho 8:6

g 1Fa 21:21

h 2Fa 13:1, 10
2Fa 14:23
2Fa 15:8, 12

i Kum 10:12
Ho 1:4

j 1Fa 12:28-30
1Fa 13:34
1Fa 14:16

Safu ya 2

a 1Fa 19:17
2Fa 8:12
2Fa 13:22

b Hes 32:33
Yos 22:9

c Kum 3:13-16
Kum 28:63
Yos 13:8-12

d 2Fa 13:1

SURA YA 11

e 2Fa 8:26
2Fa 11:20
2Nya 21:5, 6
2Nya 24:7

f 2Fa 9:27

g 2Nya 21:4
2Nya 22:10-12

h 2Fa 12:1

mbulia kotekote katika eneo la Israeli,^a **33** kuanzia Yordani kuelekea mashariki, nchi yote ya Gileadi—ya watu wa kabila la Gadi, Rubeni, na Manase^b—kutoka Aroeri, jiji lililo kando ya Bonde la Arnoni,^c mpaka Gileadi na Bashani.^c

34 Na mambo mengine katika historia ya Yehu, mambo yote aliyofanya na ukuu wake, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **35** Kisha Yehu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake huko Samaria; na Yehoahazi mwana wake^d akawa mfalme baada yake. **36** Yehu alitawala Israeli kwa miaka 28 akiwa Samaria.

11 Basi Athalia^e mama ya Ahazia alipoona kwamba mwanawe amekufa,^f alitoka na kuangamiza uzao wote wa kifalme.*^g **2** Hata hivyo, Yehosheba binti ya Mfalme Yehoram, dada ya Ahazia, akamchukua Yehoashi^h mwana wa Ahazia, akamwiba kutoka miongoni mwa wana wa mfalme walio-paswa kuuawa na kumweka yeye pamoja na mlezi wake katika chumba cha ndani cha kulala. Wakafanikiwa kumficha ili Athalia asimwone, kwa hiyo hakuuawa. **3** Akakaa pamoja naye kwa miaka sita akiwa amefichwa katika nyumba ya Yehova, Athalia alipo-kuwa akitawala nchi.

4 Katika mwaka wa saba, Yehoyada aliagiza wakuu wa mamia wa walinzi walioitwa Wakari na wa walinzi* wa ju-

10:33 *Au “Korongo la Arnoni.” 11:1 *Tnn., “mbegu yote ya ufalme.” 11:4 *Tnn., “wakimbaji.”

mba la mfalme^a waitwe, wakaja kwake katika nyumba ya Yehova. Akafanya mapatano* pamoja nao na kuwaapisha kuhusu mapatano hayo katika nyumba ya Yehova, kisha akawaonyesha mwana wa mfalme.^b **5** Akawapa agizo hili: "Hivi ndivyo mtakavyofanya: Theluthi moja watashika zamu siku ya Sabato, na kuweka ulinzi mkali katika nyumba ya* mfalme.^c **6** Theluthi nyingine watakuwa katika Lango la Msingi, na theluthi nyingine watakuwa katika lango lililo nyuma ya walinzi wa jumba la mfalme. Mtalinda nyumba hiyo kwa zamu. **7** Vikundi vyenu viwili ambavyo havipaswi kuwa na zamu siku ya Sabato vinapaswa kuweka ulinzi mkali katika nyumba ya Yehova ili kumlinda mfalme. **8** Mnapaswa kumzunguka mfalme pande zote, kila mmoja akiwa na silaha zake mikononi mwake. Yeyote atakayekaribia kikosi hicho atauawa. Mfuatani mfalme popote aendapo."*

9 Wakuu wa mamia^d waka-fanya sawasawa na alivyoamuru kuhani Yehoyada. Basi kila mmoja wao akachukua wanaume wake waliokuwa na zamu siku ya Sabato, pamoja na wale ambao hawakuwa na zamu siku ya Sabato, wakaja kwa kuhani Yehoyada.^e **10** Kisha kuhani akawapa wakuu wa mamia mikuki na ngao za mvingo zilizokuwa za Mfalme Daudi, ambazo zilikuwa katika nyumba ya Yehova. **11** Na walinzi wa jumba la mfalme^f wakasima-

11:4 *Au "agano." 11:5, 16 *Au "jumba la." 11:8 *Tnn., "anapotoka nje na anapoingia ndani."

SURA YA 11

a 1Fa 14:27

b 2Nya 23:1-3

c 1Fa 7:1
2Nya 23:4-7

d 2Fa 11:4

e 2Nya 23:8-11

f 1Fa 14:27

Safu ya 2

a 1Fa 8:22
2Nya 4:1

b 2Fa 11:2

c Kut 25:21
Kut 31:18

d 1Fa 1:39, 40

e 2Nya 23:12-15

f 2Fa 23:3

g 2Nya 5:12

h 2Fa 11:4
2Nya 23:9

i 1Fa 7:1

j 1Sa 10:25
2Sa 5:3

ma mahali pao, kila mmoja akiwa na silaha zake mikononi, kuanzia upande wa kulia wa nyumba mpaka upande wa kushoto wa nyumba, kando ya madhabahu,^a na kando ya nyumba hiyo, kumzunguka mfalme pande zote. **12** Kisha Yehoyada akamtoa nje mwana wa mfalme^b na kumvika taji na Ushahidi,^{*c} wakamweka kuwa mfalme na kumtia mafuta. Wakaanza kupiga makofi na kusema: "Mfalme na aishi muda mrefu!"^d

13 Athalia aliposikia sauti ya watu wakikimbia, mara moja akaja na kujiunga na watu katika nyumba ya Yehova.^e **14** Kisha akamwona mfalme akiwa amesimama hapo kando ya nguzo kama ilivyokuwa desturi.^f Wakuu na wapiga tarumbeta^g walikuwa pamoja na mfalme, na watu wote nchini walikuwa waki-shangilia na kupiga tarumbeta. Ndipo Athalia akayararua mavazi yake na kupaza sauti: "Ni njama! Ni njama!" **15** Lakini kuhani Yehoyada akawaamuru hivi wakuu wa mamia,^h wale waliowekwa kulisimamia jeshi: "Mwondoeni miongoni mwa vikosi, na yeyote aki-mfuata, mueni kwa upanga!" Kwa maana kuhani alikuwa amesema: "Msimuue ndani ya nyumba ya Yehova." **16** Basi wakamkamata, na alipofika mahali ambapo farasi huingia katika nyumba ya* mfalme,ⁱ akauawa hapo.

17 Kisha Yehoyada akafanya agano kati ya Yehova na mfalme na watu,^j kwamba wataendelea kuwa watu

11:12 *Labda ni kitabu cha kukunjwa kilichokuwa na Sheria ya Mungu.

wa Yehova, pia akafanya agano kati ya mfalme na watu.^a **18** Baada ya hayo, watu wote nchini wakaenda kwenye nyumba ya* Baali na kubomoa madhabahu zake,^b nao wakarivunja kabisa sanamu zake,^c na kumuua Matani kuhani wa Baali^d mbele ya madhabahu.

Halafu kuhani akawaweka waangalizi wa nyumba ya Yehova.^e **19** Tena, akawachukua wakuu wa mamia,^f walinski walioitwa Wakari, walinski wa jumba la mfalme,^g na watu wote nchini ili wamsindikize mfalme kushuka kutoka katika nyumba ya Yehova, wakaja katika jumba la mfalme kupitia lango la walinski wa jumba la mfalme. Kisha mfalme akaketi kwenye kiti cha wafalme.^h **20** Basi watu wote nchini wakashangilia na jiji likatulia, kwa maana walikuwa wame-muua Athalia kwa upanga katika jumba la mfalme.

21 Yehoashiⁱ alikuwa na umri wa miaka saba alipoanza kutawala.^j

12 Katika mwaka wa 7 wa utawala wa Yehu,^k Yehoashi^l akawa mfalme, naye akatawala kwa miaka 40 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Sibia kutoka Beer-sheba.^m **2** Yehoashi akaendelea kute-nda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova sikuzote ambazo kuhani Yehoyada alimfundisha. **3** Hata hivyo, mahali pa juuⁿ hapakuondolewa, na bado watu walikuwa wakitoa dhabihu na kufukiza moshi wa dhabihu mahali pa juu.

4 Yehoashi akawaambia makuhani: "Chukueni pesa zote zinazoletwa katika nyumba ya

11:18 *Au "hekalu la."

SURA YA 11

a 2Nya 23:16, 17

b Kum 12:3

c Kum 7:25

d Kum 13:5

e 2Nya 23:18-21

f 2Fa 11:4, 15

g 1Fa 14:27

h 2Sa 7:8, 16

i 2Fa 11:2

j 2Nya 24:1

SURA YA 12

k 1Fa 19:16

2Fa 10:30

l 2Fa 11:2

1Nya 3:10, 11

m 2Nya 24:1, 2

n Hes 33:52

Safu ya 2

a 2Nya 31:12

b Kut 30:13

2Nya 24:9

c Kut 25:2

Kut 35:21

d 2Nya 24:7

e 2Nya 24:5

f 2Fa 11:4

2Nya 23:1

2Nya 24:15

g 2Nya 24:6

h 2Nya 24:8

Mk 12:41

Lu 21:1

i 2Nya 24:10

Yehova kwa ajili ya matoleo matakatifu,^a pesa ambazo kila mtu amekadiriwa kutoa,^b pesa zilizotolewa kama thamani iliyokadiriwa ya mtu,^c na pesa zote ambazo moyo wa kila mtu umemchochea kuleta katika nyumba ya Yehova.^c **5** Makuhani wenyewe watachukua pesa hizo kutoka kwa wale wanaozitoa* na kuzitumia kurekebisha nyumba hiyo, sehemu yoyote iliyoharibika."^d

6 Kufikia mwaka wa 23 wa utawala wa Mfalme Yehoashi, makuhani walikuwa bado hawajairekebisha nyumba hiyo.^e **7** Kwa hiyo Mfalme Yehoashi akamwita kuhani^f Yehoyada na makuhani wengine na kuwauliza: "Kwa nini hamwirekebishi nyumba? Kwa hiyo msichukue pesa zaidi kutoka kwa watu ikiwa hazitumiwi kurekebisha nyumba."^g **8** Basi makuhani wakakubali kwamba hawatachukua pesa zaidi kutoka kwa watu na kwamba hawatakuwa na wajibu wa kurekebisha nyumba hiyo.

9 Kisha kuhani Yehoyada akachukua sanduku,^h akato-boa tundu kwenye kifuniko chake, akaliweka kando ya madhabahu upande wa kulia unapoingia ndani ya nyumba ya Yehova. Makuhani waliolinda mlangoni waliweka pesa zote zilizoletwa katika nyumba ya Yehova katika sanduku hilo.ⁱ **10** Kila mara walipoona kwamba sanduku hilo lina pesa nyingi, mwandishi wa mfalme na kuhani mkuu walikuja na kuzikusanya* na kuzihesabu pesa hizo zilizo-

12:4 *Au "nafsi." 12:5 *Au "wale wanaowajua." #Au "yenye nyufa." 12:10 *Au "kuziweka ndani ya mifuko." Tnn., "kuzifunga."

letwa katika nyumba ya Yehova.^a **11** Waliwapa wale walio-wekwa kusimamia kazi katika nyumba ya Yehova pesa zilizo-kuwa zimehesabiwa. Nao wakawalipa maseremala na waje-nzi waliokuwa wakifanya kazi katika nyumba ya Yehova,^b **12** na pia waashi na watu waliokata mawe. Pia walinunua mbao na mawe yaliyochongwa kwa ajili ya kurekebisha sehemu zilizoharibika za nyumba ya Yehova na kutumia pesa hizo kulipia gharama nyingi-ne zote za kurekebisha nyumba hiyo.

13 Hata hivyo, hawakutumia pesa zozote zilizole-twa katika nyumba ya Yehova kutengeneza mabeseni ya fedha, mikasi ya kukatia tamba za taa, mabakuli, tarumbeta,^c au kitu chochote cha dhahabu au fedha kwa ajili ya nyumba ya Yehova.^d **14** Waliwapa pesa hizo wale tu waliofanya kazi hiyo, nao walizitumia kurekebisha nyumba ya Yehova. **15** Hawakudai hesabu ya matumizi ya pesa hizo kutoka kwa wanaume walio-wapa pesa za kuwalipa wafanyakazi, kwa sababu wanaume hao walikuwa waaminifu.^e **16** Hata hivyo, pesa za dhambi-hu za hatia^f na pesa za dhambi-hu za dhambi hazikuletwa katika nyumba ya Yehova; zilikuwa za makuhani.^g

17 Wakati huo ndipo Hazaeli^h mfalme wa Siria alipanda kwenda kupigana na jiji la Gathi,ⁱ naye akaliteka, kisha akaamua kulishambulia* jiji la Yerusalemu.^j **18** Ndipo Mfalme Yehoashi wa Yuda akachu-

12:17 *Tnn., "Hazaeli akauelekeza uso wake dhidi ya."

SURA YA 12

a 2Nya 24:11

b 2Fa 22:4-6
2Nya 24:12c Hes 10:2
2Nya 5:12

d 2Nya 24:14

e 2Fa 22:7

f Law 5:15

g Law 7:7
Hes 18:8h 1Fa 19:15
2Fa 8:13
2Fa 10:32

i 1Nya 18:1

j 2Nya 24:23

Safu ya 2

a 1Fa 15:18
2Fa 16:8
2Fa 18:15b 2Nya 24:25, 26
2Nya 25:27c 2Sa 5:9
1Fa 9:15, 24
2Nya 32:5

d 2Fa 14:1, 5

e 2Nya 24:27

SURA YA 13

f 2Fa 11:2, 21

g 2Fa 8:26
2Fa 9:27

h 2Fa 10:30, 35

i 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33
1Fa 14:16

j Ebr 12:29

k Law 26:14, 17

kua matoleo yote matakatiifu ambayo mababu zake Yehoshafati, Yehoram, na Ahazia, wafalme wa Yuda, walikuwa wameyatakaswa na pia matoleo yake mwenyewe matakatiifu na dhahabu yote iliyokuwa katika hazina za nyumba ya Yehova na katika nyumba ya mfalme,* akampelekea Hazaeli mfalme wa Siria.^a Kwa hiyo Hazaeli akaondoka Yerusalemu.

19 Na mambo mengine katika historia ya Yehoashi, mambo yote aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha nyakati za wafalme wa Yuda? **20** Hata hivyo, watumishi wake walipanga njama dhidi ya Yehoashi^b na kumuua katika nyumba ya Kilima,^c katika njia inayoshuka kwenda Sila. **21** Yozakari mwana wa Shimeathi na Yehozabadi mwana wa Shomeri, watumishi wake, ndio waliompiga na kumuua.^d Wakamzika pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi, na Amazia mwanawe akawa mfalme baada yake.^e

13 Katika mwaka wa 23 wa utawala wa Yehoashi^f mwana wa Ahazia^g mfalme wa Yuda, Yehoahazi mwana wa Yehu^h akawa mfalme wa Israeli huko Samaria, naye alitawala kwa miaka 17. **2** Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, na kuendelea kutenda dhambi ya Yeroboamu mwana wa Nebati aliyosababisha Waisraeli kutenda.ⁱ Hakugeuka na kuiacha. **3** Kwa hiyo hasira ya Yehova^j ikawaka dhidi ya Waisraeli,^k akawatia mikononi mwa Mfalme

12:18 *Au "jumba la mfalme." 12:20 *Au "Beth-milo."

Hazaeli^a wa Siria na mikononi mwa Ben-hadadi^b mwana wa Hazaeli siku zao zote.

4 Baada ya muda Yehoahazi akamsihi Yehova amwonyeshe kibali,* naye Yehova akamsikiliza, kwa maana alikuwa ameona jinsi mfalme wa Siria alivyowakandamiza Waisraeli.^c **5** Basi Yehova akawapa Waisraeli mwokozi^d ili awaokoe kutoka mikononi mwa Wasiria, na Waisraeli wakakaa katika nyumba zao kama awali.* **6** (Hata hivyo, hawakuacha dhambi ya nyumba ya Yeroboamu aliyosababisha Waisraeli kutenda.^e Waliendelea kutenda* dhambi hiyo, na mti mtakatifu^{ff} ukandelea kusimama huko Samaria.) **7** Yehoahazi akabaki tu na jeshi lenye wapanda farasi 50, magari 10 ya vita, na wanajeshi 10,000 wanaotembea kwa miguu kwa sababu mfalme wa Siria alikuwa ame-waangamiza,^g aliwakanyagakanyaga kama mavumbi wakati wa kupura.^h

8 Na mambo mengine katika historia ya Yehoahazi, mambo yote aliyofanya na ukuu wake, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **9** Kisha Yehoahazi akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake huko Samaria;ⁱ na Yehoashi mwanawe akawa mfalme baada yake.

10 Katika mwaka wa 37 wa utawala wa Mfalme Yehoashi wa Yuda, Yehoashi^j mwana wa Yehoahazi akawa mfalme wa Israeli huko Sama-

13:4 *Au "akautuliza uso wa Yehova."
13:5 *Yaani, kwa amani na usalama.
13:6 *Tnn., "Aliendelea kutembea katika." ^aAngalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 13

a 1Fa 19:17
 2Fa 8:12

b 2Fa 13:24

c Kut 3:7
 Amu 10:16
 2Fa 14:26, 27

d Ne 9:27

e 2Fa 10:29
 2Fa 17:21

f Kum 7:5
 1Fa 14:15
 1Fa 16:33

g 2Fa 8:12
 2Fa 10:32

h Amo 1:3

i 2Fa 10:35

j 2Fa 14:1

Safu ya 2

a 2Fa 10:29

b 2Fa 14:8,13

c 2Fa 14:28

d 2Fa 10:35
 2Fa 13:9

e 1Fa 19:16

f 2Fa 2:11,12

ria, naye alitawala kwa miaka 16. **11** Akaendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, hakuacha kutenda dhambi zote za Yeroboamu mwana wa Nebati alizosababisha Waisraeli kutenda.^a Aliendelea kutenda* dhambi hizo.

12 Na mambo mengine katika historia ya Yehoashi, mambo yote aliyofanya na ukuu wake na jinsi alivyopigana na Mfalme Amazia wa Yuda,^b je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **13** Kisha Yehoashi akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake, na Yeroboamu^{*c} akaketi kwenye kiti chake cha ufalme. Naye Yehoashi akazikwa huko Samaria pamoja na wafalme wa Israeli.^d

14 Sasa Elisha^e alipougua ugonjwa ambao hatimaye ulisababisha kifo chake, Yehoashi mfalme wa Israeli alishuka kwenda kwake na kumlilia akisema: "Baba yangu, baba yangu! Gari la vita la Israeli na wapanda farasi wake!"^f **15** Ndipo Elisha akamwambia: "Chukua upinde na mishale." Basi akachukua upinde na mishale. **16** Kisha akamwambia mfalme wa Israeli: "Shika upinde wako." Basi akashika upinde wake, halafu Elisha akaweka mikono yake juu ya mikono ya mfalme. **17** Kisha akasema: "Fungua dirisha la upande wa mashariki." Basi akalifungua. Elisha akasema: "Piga mshale!" Basi akapiga mshale. Sasa akasema: "Mshale wa ushindi* wa

13:11 *Tnn., "Alitembea katika." **13:13** *Yaani, Yeroboamu wa Pili. **13:17** *Au "wokovu."

Yehova, mshale wa ushindi* dhidi ya Siria! Utapiga[#] Siria huko Afeki^a mpaka uangamimize kabisa.”

18 Akaendelea kusema: “Chukua mishale,” naye akai-chukua. Kisha Elisha akamwambia mfalme wa Israeli: “Piga ardhi.” Basi akapiga ardhi mara tatu halafu akaacha.

19 Ndipo yule mtu wa Mungu wa kweli akamkasirikia sana na kumwambia: “Ulipaswa kuipiga ardhi mara tano au mara sita! Kama ungefanya hivyo, ungeipiga Siria mpaka uangamimize, lakini sasa utaipiga Siria mara tatu tu.”^b

20 Baada ya hayo, Elisha akafa na kuzikwa. Kuli-kuwa na makundi ya wavamizi^c ya Wamoabu yaliyokuwa yakija nchini mwanzoni mwa mwaka.* **21** Wanaume fulani walipokuwa wakimzika mtu, waliona kundi la wavamizi, kwa hiyo wakamtupa mara moja mtu huyo ndani ya kaburi la Elisha na kukimbia. Mtu huyo alipogusa mifupa ya Elisha, akafufuka^d na kusimama.

22 Sasa Mfalme Hazaeli^e wa Siria aliwakandamiza Waisraeli^f sikuzote za utawala wa Yehoahazi. **23** Hata hivyo, Yehova akawaonyesha kibali na rehema^g na kuwajali kwa sababu ya agano lake na Abrahamu,^h Isaka,ⁱ na Yakobo.^j Hakutaka kuwaangamiza, naye hajawatupa mbali kutoka mbele zake* mpaka leo. **24** Mfalme Hazaeli wa Siria alipokufa, Ben-hadadi mwana-we akawa mfalme baada yake.

13:17 *Au “wokovu.” [#]Au “Utaishinda.” 13:20 *Tnn., “mwaka unapoingia,” inawezekana ni wakati wa masika. 13:23 *Tnn., “kutoka kwenye uwepo wake.”

SURA YA 13

a 1Sa 29:1
1Fa 20:26

b 2Fa 13:25

c 2Fa 1:1
2Fa 24:2

d Yoh 11:44
Ebr 11:35

e 1Fa 19:15

f 2Fa 8:12
2Fa 10:32

g 2Fa 14:26, 27

h Mwa 13:14-16

i Mwa 26:3

j Mwa 28:13
Zb 105:8
Mik 7:20

Safu ya 2

a 2Fa 13:19

SURA YA 14

b 2Fa 13:10

c 2Nya 25:1-4

d 1Fa 15:5

e 2Nya 24:2

f 1Fa 15:14

g 2Fa 12:1, 3

h 2Fa 12:20
2Nya 24:25

i Kum 24:16

j 2Fa 8:20

k 2Sa 8:13
1Nya 18:12

l 2Nya 25:11, 12

25 Kisha Yehoashi mwana wa Yehoahazi akayachukua tena majiji ambayo Ben-hadadi mwana wa Hazaeli alikuwa ameyachukua vitani kutoka kwa Yehoahazi baba yake. Yehoashi alimshinda Ben-hadadi mara tatu,^a naye akayakomboza majiji ya Israeli.

14 Katika mwaka wa pili wa utawala wa Yehoashi^b mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli, Amazia mwana wa Mfalme Yehoashi wa Yuda akawa mfalme.

2 Alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 29 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Yehoadini wa Yerusalemu.^c

3 Aliendelea kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova, lakini si kama Daudi^d babu yake. Alifanya mambo yote kama Yehoashi baba yake.^e

4 Hata hivyo, mahali pa juu hapakuondolewa,^f na watu bado walikuwa wakitoa dhabihu na kufukiza moshi wa dhabihu katika mahali pa juu.^g

5 Mara tu ufalme ulipoimarika kabisa mikononi mwake, aliwaua watumishi wake waliomua mfalme, baba yake.^h

6 Lakini hakuwaua wana wa wauaji hao, kulingana na amri hii ya Yehova iliyoandikwa katika kitabu cha Sheria ya Musa: “Akina baba hawapaswi kuuawa kwa sababu ya wana wao, na wana hawapaswi kuuawa kwa sababu ya baba zao; lakini kila mtu anapaswa kuuawa kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe.”ⁱ

7 Akawaua Waedomu^j katika Bonde la Chumvi,^k wanaume 10,000, akaliteka jiji la Sela katika vita hivyo,^l na

tangu wakati huo jiji hilo likaitwa Yoktheeli.

8 Kisha Amazia akawatuma wajumbe kwa Yehoashi mwana wa Yehoahazi mwana wa Yehu mfalme wa Israeli, aki-sema: “Njoo, tupambane vitani.”*^a **9** Mfalme Yehoashi wa Israeli akatuma ujumbe huu kwa Mfalme Amazia wa Yuda: “Gugu lenye miiba kule Lebanoni lilituma ujumbe huu kwa mwerezi huko Lebanoni, ‘Mpe mwanangu binti yako awe mke wake.’ Hata hivyo, mnyama wa mwituni wa Lebanoni akapita karibu na kulikanyaga-kanyaga gugu hilo lenye miiba. **10** Ni kweli kwamba uliwaangamiza Waedomu,^b kwa hiyo moyo wako umekuwa na kiburi. Furahia utukufu wako, lakini kaa katika nyumba yako mwenyewe.* Kwa nini utafute msiba kisha uanguke, na ku-waangusha pia watu wa Yuda?” **11** Lakini Amazia hakusikiliza.^c

Basi Mfalme Yehoashi wa Israeli akapanda kwenda huko, naye akapambana vitani na Mfalme Amazia wa Yuda huko Beth-shemesh,^d jiji la Yuda.^e **12** Watu wa Yuda wakashindwa na Waisraeli, kwa hiyo kila mmoja akakimbilia nyumbani kwake.* **13** Mfalme Yehoashi wa Israeli akamkamata Mfalme Amazia wa Yuda, mwana wa Yehoashi mwana wa Ahazia, huko Beth-shemesh. Kisha wakaja Yerusalemu, naye akabomoa ukuta wa Yerusalemu kuanzia Lango la Efraimu^f mpaka Lango la Pembeni,^g urefu wa mi-

14:8 *Au “tukutane uso kwa uso.”

14:10 *Au “jumba lako la mfalme.”

14:12 *Tnn., “katika hema lake.”

SURA YA 14

a 2Nya 25:17-19

b 2Fa 14:7

c 2Nya 25:15, 16

d Yos 15:10, 12
Yos 21:8, 16

e 2Nya 25:20-24

f Ne 8:16
Ne 12:38, 39

g Yer 31:38
Zek 14:10

Safu ya 2

a 2Fa 10:35
2Fa 13:9

b Ho 1:1
Amo 1:1
Amo 7:10

c 2Fa 14:1

d 2Fa 13:10

e 2Nya 25:25-28

f 2Fa 12:20

g 1Fa 2:10

h Mt 1:8

kono 400.* **14** Akachukua dhahabu yote na fedha na vitu vyote vilivyokuwa katika nyumba ya Yehova na katika hazina za nyumba ya mfalme,* na pia akachukua mateka. Kisha akarudi Samaria.

15 Na mambo mengine katika historia ya Yehoashi, mambo aliyofanya na ukuu wake na jinsi alivyopigana na Mfalme Amazia wa Yuda, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? **16** Kisha Yehoashi akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake huko Samaria^a pamoja na wafalme wa Israeli; na Yeroboamu mwana wake*^b akawa mfalme baada yake.

17 Amazia^c mwana wa Yehoashi mfalme wa Yuda aliendelea kuishi kwa miaka 15 baada ya kifo cha Yehoashi^d mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli.^e **18** Na mambo mengine katika historia ya Amazia, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **19** Baadaye njama ikapangwa dhidi yake^f huko Yerusalemu, naye akakimbilia Lakishi, lakini wakawatumu watu wamfuatie huko Lakishi, nao wakamuuu huko. **20** Kwa hiyo wakambeba juu ya farasi, naye akazikwa Yerusalemu pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.^g **21** Kisha watu wote wa Yuda wakamchukua Azaria,^{*h} aliyeye-

14:13 *Karibu mita 178 (futi 584). Angalia Nyongeza B14. **14:14** *Au “jumba la mfalme.” **14:16** *Yaani, Yero-boamu wa Pili. **14:21** *Maana yake “Yehova Amesaidia.” Anaitwa Uzia katika 2Fa 15:13; 2Nya 26:1-23; Isa 6:1; na Zek 14:5.

kuwa na umri wa miaka 16,^a wakamweka kuwa mfalme baada ya Amazia baba yake.^b

22 Alijenga upya jiji la Elathi^c na kulirudisha kwa Yuda baada ya mfalme* kuzikwa pamoja na mababu zake.^d

23 Katika mwaka wa 15 wa utawala wa Amazia mwana wa Yehoashi mfalme wa Yuda, Yeroboamu^e mwana wa Mfalme Yehoashi wa Israeli akawa mfalme huko Samaria, naye alitawala kwa miaka 41.

24 Aliendelea kutenda mao-vu machoni pa Yehova. Hakuacha dhambi zote za Yeroboamu mwana wa Nebati ambazo alisababisha Waisraeli kutenda.^f **25** Alirudisha mpaka wa Israeli kuanzia Lebo-hamathi^g hadi kwenye Bahari ya Araba,^h kulingana na neno ambalo Yehova Mungu wa Israeli alisema kupitia Yonaⁱ mtumishi wake, mwana wa Amitai, nabii kutoka Gath-heferi.^j **26** Kwa maana Yehova alikuwa ameyaona mate-so makali sana ya Waisraeli,^k Hakukuwa na yeyote aliyebaki wa kuwasaidia Waisraeli, hata watu wasio na uwezo au walio dhaifu hawakuwepo. **27** Lakini Yehova alikuwa ameahidi kwamba hatafutulia mbali jina la Israeli kutoka chini ya mbingu.^l Kwa hiyo akawao-koa kwa mkono wa Yeroboamu mwana wa Yehoashi.^m

28 Na mambo mengine katika historia ya Yeroboamu, mambo yote aliyofanya na ukuu wake, jinsi alivyopigana na jinsi alivyorudisha jiji la Damaskoⁿ na Hamathi^o ili yamilikiwe tena na Yuda nchi-

14:22 *Yaani, Amazia baba yake.

14:25 *Au "nija ya kuingia Hamathi."
#Yaani, Bahari ya Chumvi.

SURA YA 14

a 2Fa 15:1, 2

b 2Nya 26:1

c Kum 2:8
1Fa 9:26
2Fa 16:6

d 2Nya 26:2

e Ho 1:1
Amo 1:1f 1Fa 12:28-30
1Fa 13:34
Zb 106:20g Hes 13:21
Hes 34:2, 7, 8

h Kum 3:16, 17

i Yon 1:1
Mt 12:39

j Yos 19:10, 13

k Kut 3:7
Amu 10:16
Zb 106:43, 44

l Yer 31:20

m 2Fa 13:4, 5

n 2Sa 8:6

o 2Nya 8:3

Safu ya 2

a 2Fa 15:8

SURA YA 15

b 2Fa 14:21

c 2Fa 14:1

d 2Nya 26:1, 3

e 2Nya 26:4, 5

f Hes 33:52

g Kum 12:13, 14
1Fa 22:41, 43
2Fa 14:1, 4h Hes 12:10
2Fa 5:27

i Law 13:45, 46

j 2Fa 15:32

k 2Nya 26:16-21

l 2Nya 26:22, 23

m Isa 6:1

ni Israeli, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli?

29 Kisha Yeroboamu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake, pamoja na wafalme wa Israeli; na Zekaria^a mwanawe akawa mfalme baada yake.

15 Katika mwaka wa 27 wa utawala wa Mfalme Yeroboamu* wa Israeli, Azaria^{#b} mwana wa Mfalme Amazia^c wa Yuda akawa mfalme.^d **2** Alikuwa na umri wa miaka 16 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 52 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Yekolia wa Yerusalemu.

3 Aliendelea kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova, kama alivyotenda Amazia baba yake.^e **4** Hata hivyo, mahali pa juu hapakuondolewa,^f na watu bado walikuwa wakitoa dhahibu na kufukiza moshi wa dhahibu mahali pa juu.^g **5** Yehova alimletea mfalme pigo, naye aliendelea kuwa na ukoma^h mpaka siku aliyokufa; alikaa katika nyumba iliyotengwa,ⁱ huku Yothamu mwana wa mfalme^j akiisimamia nyumba ya mfalme,* akiwahukumu watu nchini.^k

6 Na mambo mengine katika historia ya Azaria,^l mambo yote aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **7** Kisha Azaria akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake^m katika Jiji la Daudi; na Yothamu mwanawe akawa mfalme baada yake.

15:1 *Yaani, Yeroboamu wa Pili. #Maana yake "Yehova Amesaidia." Anaitwa Uzia katika 2Fa 15:13; 2Nya 26:1-23; Isa 6:1; na Zek 14:5. 15:5 *Au "jumba la mfalme."

8 Katika mwaka wa 38 wa utawala wa Mfalme Azaria^a wa Yuda, Zekaria^b mwana wa Yeroboamu akawa mfalme wa Israeli huko Samaria, naye alitawala kwa miezi sita. 9 Alitenda maovu machoni pa Yehova, kama wali-vyotenda mababu zake. Hakuacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati alizosababisha Waisraeli kutenda.^c 10 Kisha Shalumu mwana wa Yabeshi akapanga njama dhidi yake na kumuua^d huko Ibleamu.^e Baada ya kumuua, Shalumu akawa mfalme. 11 Na mambo mengine katika historia ya Zekaria yameandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli. 12 Hilo lilitimiza neno hili la Yehova alilokuwa amemwambia Yehu: "Vizazi vinne vya wana wako^f vitaketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli."^g Na ikawa hivyo.

13 Shalumu mwana wa Yabeshi akawa mfalme katika mwaka wa 39 wa utawala wa Mfalme Uzia^h wa Yuda, naye alitawala kwa mwezi mmoja kamili huko Samaria. 14 Kisha Menahemu mwana wa Gadi akapanda kutoka Tirsaⁱ na kuja Samaria, akamuua Shalumu^j mwana wa Yabeshi huko Samaria. Baada ya kumuua, akawa mfalme. 15 Mambo mengine katika historia ya Shalumu na njama aliyopanga, yameandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli. 16 Wakati huo ndipo Menahemu alipokuja kutoka Tirsa na kuliangamiza jiji la Tifsa na wote waliokuwa katika jiji hilo na katika eneo lake, kwa sababu hawakumfungulia mala-

SURA YA 15

a 2Fa 14:21

b 2Fa 14:29

c 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33
1Fa 14:16d Ho 1:4
Amo 7:9

e Yos 17:11

f 2Fa 13:1,10
2Fa 14:23, 29

g 2Fa 10:30

h 2Nya 26:1

i 1Fa 14:17
1Fa 15:21
1Fa 16:8, 17

j 2Fa 15:10

Safu ya 2

a 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33
1Fa 14:16

b 1Nya 5:26

c 2Fa 12:18
2Fa 16:8

d 2Fa 23:35

e 2Fa 15:14

ngo ya jiji hilo. Aliliangamiza na kuwapasua tumbo wanawake wenye mimba wa jiji hilo.

17 Katika mwaka wa 39 wa utawala wa Mfalme Azaria wa Yuda, Menahemu mwana wa Gadi akawa mfalme wa Israeli, naye alitawala kwa miaka kumi huko Samaria. 18 Aliendelea kute nda maovu machoni pa Yehova. Na sikuzote za utawala wake hakuacha dhambi zote za Yeroboamu mwana wa Nebati alizosababisha Waisraeli kutenda.^a 19 Mfalme Pulu^b wa Ashuru aliingia nchini, na Menahemu akampa Pulu talanta 1,000 za fedha* ili amsaidie kuimarisha mamlaka yake katika ufalme huo.^c 20 Kwa hiyo Menahemu alikusanya fedha hizo kwa kuwatoza ushuru wanaume mashuhuri na matajiri wa Israeli.^d Akampa mfalme wa Ashuru shekeli 50 za fedha* kwa kila mwanamume. Kisha mfalme wa Ashuru akarudi, hakukaa nchini. 21 Na mambo mengine katika historia ya Menahemu,^e mambo yote aliyofanya, je, hayaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli? 22 Kisha Menahemu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake; na Pekahia mwana wake akawa mfalme baada yake.

23 Katika mwaka wa 50 wa utawala wa Mfalme Azaria wa Yuda, Pekahia mwana wa Menahemu akawa mfalme wa Israeli huko Samaria, naye alitawala kwa miaka miwili.

15:19 * Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.
15:20 * Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

24 Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova. Hakuacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati alizosababisha Waisraeli kutenda.^a

25 Kisha Peka^b mwana wa Remalia kamanda wake msaidizi akapanga njama dhidi yake na kumuua huko Samaria katika mnara wenye ngo-me wa nyumba ya mfalme* pamoja na Argobu na Arie. Alikuwa pamoja na wanaume 50 wa Gileadi; na baada ya kumuua, akawa mfalme. **26** Na mambo mengine katika historia ya Pekahia, mambo yote aliyofanya, yameandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli.

27 Katika mwaka wa 52 wa utawala wa Mfalme Azaria wa Yuda, Peka^c mwana wa Remalia akawa mfalme wa Israeli huko Samaria, naye alitawala kwa miaka 20. **28** Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, naye hakuacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati alizosababisha Waisraeli kutenda.^d

29 Katika siku za utawala wa Mfalme Peka wa Israeli, Mfalme Tiglath-pileseri^e wa Ashuru alivamia na kuteka Iyoni, Abel-beth-maaka,^f Yanoa, Kedeshi, Hasori, Gileadi,^g na Galilaya,^h nchi yote ya Naftali,ⁱ akawapeleka wakaaji wa maeneo hayo uhamishoni kule Ashuru.^j **30** Kisha Hoshea^k mwana wa Ela akapanga njama dhidi ya Peka mwana wa Remalia, akampiga na kumuua; naye akawa mfalme baada yake katika mwaka wa 20 wa utawala wa Yothamu^l mwana wa Uzia.

15:25 *Au "jumba la mfalme."

SURA YA 15

a 1Fa 12:28-30

1Fa 13:33
1Fa 14:16

b 2Nya 28:6

c 2Nya 28:6

Isa 7:1, 4

d 1Fa 12:28-30

1Fa 13:33
1Fa 14:16

e 2Fa 16:7

1Nya 5:6
1Nya 5:26
2Nya 28:19, 20

f 1Fa 15:20

g Yos 20:7, 9

h Isa 9:1

i Hes 32:40

j Law 26:38

Kum 28:64
2Fa 17:22, 23
Isa 8:4

k 2Fa 17:1

l 2Nya 27:1

Safu ya 2

a 2Nya 27:7

Mt 1:9

b 2Fa 14:21

c 2Nya 27:1

d 2Nya 27:2

e Hes 33:52

Kum 12:14

f 2Nya 27:3

g 2Fa 15:27

2Nya 28:6

h 2Fa 16:5

Isa 7:1, 2

SURA YA 16

i Isa 1:1

Isa 7:1

Ho 1:1

Mik 1:1

Mt 1:9

31 Na mambo mengine katika historia ya Peka, mambo yote aliyofanya, yameandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Israeli.

32 Katika mwaka wa pili wa utawala wa Peka mwana wa Remalia mfalme wa Israeli, Yothamu^a mwana wa Mfalme Uzia^b wa Yuda akawa mfalme.

33 Alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 16 huko Yerusalemu. Mama yake alii-twa Yerusha binti ya Sadoki.^c

34 Aliendelea kutenda yali-yokuwa sawa machoni pa Yehova, kama aliyofanya Uzia baba yake.^d **35** Hata hivyo, mahali pa juu hapakuondolewa, na watu bado walikuwa wakitoa dhabihu na kufukiza moshi wa dhabihu mahali pa juu.^e Yeye ndiye aliyeje-nga lango la juu la nyumba ya Yehova.^f **36** Na mambo mengine katika historia ya Yothamu, mambo aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **37** Siku hizo Yehova alianza kumtuma Resini mfalme wa Siria na Peka^g mwana wa Remalia kushambulia Yuda.^h **38** Kisha Yothamu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi babu yake. Na Ahazi mwanawe akawa mfalme baada yake.

16 Katika mwaka wa 17 wa utawala wa Peka mwana wa Remalia, Ahaziⁱ mwana wa Mfalme Yothamu wa Yuda akawa mfalme.

2 Ahazi alikuwa na umri wa miaka 20 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 16 huko Yerusalemu. Hakute-nda yaliyokuwa sawa machoni

pa Yehova Mungu wake, kama alivyotenda Daudi babu yake.^a

3 Badala yake, alitembea katika njia ya wafalme wa Israeli,^b na hata alimteketeza* motoni mwana wake mwenyewe,^c akifuata mazoea yenye kuchukiza ya mataifa^d ambayo Yehova alikuwa ameyafukuza kutoka mbele ya Waisraeli. **4** Aliendelea pia kutoa dhahabu na kufukiza moshi wa dhahabu mahali pa juu,^e kwenye vilima, na chini ya kila mti wenye majani mengi.^f

5 Wakati huo ndipo Mfalme Resini wa Siria na Peka mwana wa Remalia mfalme wa Israeli walipopanda ili kuja kupigana vita dhidi ya Yerusalemu.^g Wakamzingira Ahazi lakini hawakuweza kuliteka jiji. **6** Wakati huo Mfalme Resini wa Siria akarudisha Elathi^h kwa Edomu, kisha akawafukuza Wayahudi* kutoka Elathi. Na Waedomu wakaingia Elathi, nao wamekuwa wakiishi humo tangu wakati huo. **7** Kwa hiyo Ahazi akatuma wajumbe kwa Mfalme Tiglath-pileseriⁱ wa Ashuru, akisema: "Mimi ni mtumishi wako na mwanao. Njoo unio- koe kutoka mikononi mwa mfalme wa Siria na kutoka mikononi mwa mfalme wa Israeli, wanaonishambulia." **8** Kisha Ahazi akachukua fedha na dhahabu iliyokuwa katika nyumba ya Yehova na katika hazina za nyumba ya mfalme,* akampelekea mfalme wa Ashuru kama rushwa.^j **9** Mfalme wa Ashuru akakubali ombi lake, naye akapanda

16:3 *Tnn., "alimpitisha." 16:6 *Au "watu wa Yuda." 16:8 *Au "jumba la mfalme."

SURA YA 16

a 2Nya 28:1-4

b 1Fa 12:28-30
1Fa 16:33c Law 20:2, 3
2Nya 33:1, 6
Yer 7:31

d Kum 12:29-31

e Hes 33:52

f Kum 12:2

g 2Fa 15:37
2Nya 28:5, 6

h 2Fa 14:21, 22

i 2Fa 15:29

j 1Fa 15:18, 19

Safu ya 2

a Amo 1:4, 5

b Isa 9:11

c Kum 12:30

d Isa 8:2

e Yer 23:11
Eze 22:26f 2Nya 28:22, 23
2Nya 28:25

g 2Nya 4:1

h Isa 8:2

i 2Nya 28:23

j Kut 29:39-41

kwenda Damasko na kuliteka jiji hilo na kuwapeleka watu wake uhamishoni huko Kiri,^a akamuua Resini.^b

10 Ndipo Mfalme Ahazi akaenda kukutana na Mfalme Tiglath-pileseri wa Ashuru kule Damasko. Alipoona madhabahu iliyokuwa Damasko, Mfalme Ahazi akamtumia kuhani Uriya ramani ya madhabahu hiyo, akamwonyesha mfano wake na jinsi ilivyojengwa.^c **11** Kuhani Uriya^d akajenga madhabahu^e kulingana na maagizo yote ambayo Mfalme Ahazi alikuwa ametuma kutoka Damasko. Kuhani Uriya akamaliza kuijenga kabla ya Mfalme Ahazi kurudi kutoka Damasko. **12** Mfalme aliporudi kutoka Damasko na kuiona madhabahu hiyo, aliikaribia na kutoa dhahabu juu yake.^f **13** Akaendelea kufukizia moshi wa dhahabu zake za kuteketezwa na matoleo yake ya nafaka juu ya madhabahu hiyo; pia aliimiminia madhabahu hiyo matoleo yake ya kinywaji na kuinyunyizia damu ya dhahabu zake za ushirika. **14** Kisha akaiondoa madhabahu ya shaba^g iliyokuwa mbele za Yehova, kutoka mahali ilipokuwa mbele ya nyumba, katikati ya madhabahu yake na nyumba ya Yehova, akaiweka upande wa kaskazini wa madhabahu yake. **15** Mfalme Ahazi akamwamuru hivi kuhani Uriya:^h "Fukiza moshi wa dhahabu ya asubuhi kwenye madhabahu hiyo kubwa,ⁱ pia toleo la nafaka la jioni,^j dhahabu ya kuteketezwa ya mfalme, na toleo lake la nafaka, na pia dhahabu za kuteketezwa, matoleo ya na-

faka, na matoleo ya kinywaji ya watu wote. Unapaswa pia kuinunyizia madhabahu hiyo damu yote ya dhahabu za kuteketezwa na damu yote ya dhahabu nyingine. Nitaamua nitakalofanya na madhabahu ya shaba.” **16** Kuhani Uriya akafanya mambo yote ambayo Mfalme Ahazi aliamuru.^a

17 Zaidi ya hayo, Mfalme Ahazi akazikata vipandevipande kuta za pembeni za yale magari^b na kuondoa mabeseni yaliyokuwa juu yake,^c akaiondoa ile Bahari kutoka juu ya wale ng’ombe dume wa shaba^d na kuiweka kwenye sakafu ya mawe.^e **18** Pia, alihamisha kutoka katika nyumba ya Yehova sehemu iliyofunikwa ambayo ilikuwa imejengwa katika nyumba hiyo kwa ajili ya Sabato na pia njia ya nje aliyotumia mfalme kuingia katika nyumba hiyo; alifanya hivyo kwa sababu ya mfalme wa Ashuru.

19 Na mambo mengine katika historia ya Ahazi, mambo aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda?^f **20** Kisha Ahazi akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi; na Hezekia^{*g} mwanawe akawa mfalme baada yake.

17 Katika mwaka wa 12 wa utawala wa Mfalme Ahazi wa Yuda, Hoshea^h mwana wa Ela akawa mfalme wa Israeli huko Samaria; alitawala kwa miaka tisa. **2** Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, lakini si kwa kiwango ambacho wafalme wa

16:20 *Maana yake “Yehova Huimarisha.”

SURA YA 16

a 2Fa 16:11

b 1Fa 7:27, 28

c 1Fa 7:38
2Nya 4:6

d 1Fa 7:23, 25

e 2Nya 28:24
2Nya 29:19

f 2Nya 28:26, 27

g 2Fa 18:1
2Nya 29:1
Isa 1:1
Ho 1:1
Mt 1:9

SURA YA 17

h 2Fa 15:30

Safu ya 2

a 2Fa 18:9
Isa 10:5, 6
Ho 10:14, 15

b 2Fa 18:14

c Isa 31:1

d Ho 13:16

e Law 26:32, 33
Kum 4:27
Kum 28:64
1Fa 14:15

f 1Nya 5:26

g 2Fa 18:9-11

h Kut 20:2

i Kut 20:5

j Ho 12:11

Israeli waliomtangulia walitenda. **3** Mfalme Shalmanesa wa Ashuru alipanda kuja kumshambulia,^a na Hoshea akawa mtumishi wake, akaanza kumlipa ushuru.^b **4** Hata hivyo, mfalme wa Ashuru alipata habari kwamba Hoshea alishiriki kupanga njama fulani, kwa maana alikuwa amewatuma wajumbe kwa Mfalme So wa Misri^c na hakuleta ushuru kwa mfalme wa Ashuru kama alivyofanya miaka iliyotangulia. Kwa hiyo, mfalme wa Ashuru akamfunga na kumtia gerezani.

5 Mfalme wa Ashuru aliiyamia nchi nzima, naye akaaja Samaria na kulizingira kwa miaka mitatu. **6** Katika mwaka wa tisa wa utawala wa Hoshea, mfalme wa Ashuru aliliteka jiji la Samaria.^d Kisha akawapeleka Waisraeli uhamishoni^e kule Ashuru na kuwaweka katika eneo la Hala na Habori kando ya mto Gozani^f na katika majiji ya Wamedi ili waishi humo.^g

7 Hilo lilitendeka kwa sababu Waisraeli walimtendea dhambi Yehova Mungu wao, aliye-watoa nchini Misri kutoka mikononi mwa Farao mfalme wa Misri.^h Waliabudu* miungu mingine,ⁱ **8** wakafuata desturi za mataifa ambayo Yehova alikuwa ameyafukuza kutoka mbele ya Waisraeli, nao wakafuata desturi zilizoanzishwa na wafalme wa Israeli.

9 Waisraeli walikuwa wakifuatia mambo ambayo hayakuwa sawa machoni pa Yehova Mungu wao. Wakaendelea kujenga mahali pa juu katika majiji yao yote,^j kuanzia

17:7 *Tnn., “Waliogopa.”

mnara wa walinzi mpaka jiji lenye ngome.* **10** Wakae-ndelea kujisimamishia nguzo takatifu na miti mitakati-fu*^a juu ya kila kilima kirefu na chini ya kila mti we-nye majani mengi;^b **11** nao walikuwa wakifukiza moshi wa dhabihu mahali pote pa juu kama yalivyofanya ma-taifa ambayo Yehova alikuwa ameyapeleka uhamishoni ku-toka mbele yao.^c Waliendelea kutenda maovu na kumkasiri-sha Yehova.

12 Waliendelea kuabudu sa-namu zenye kuchukiza,*^d ambazo Yehova alikuwa ame-waambia hivi kuzihusu: “Msi-fanye hivyo!”^e **13** Yehova ali-waonya Waisraeli na watu wa Yuda tena na tena kupitia ma-nabii wake wote na kila mwonaji,^f akisema: “Geuke-ni na kuacha njia zenu ovu!”^g Shikeni amri zangu na maa-gizo yangu kulingana na she-ria yote niliyowaamuru maba-bu zenu na ambayo niliwa-pa kupitia watumishi wangu ma-nabii.” **14** Lakini hawakusi-kiliza, nao wakaendelea kuwa wakaidi kama* mababu zao ambao hawakudhihirisha imani katika Yehova Mungu wao.^h **15** Waliendelea kukataa ma-sharti yake na agano lake! ali-lofanya na mababu zao na vi-kumbusho vyake alivyowapa ili kuwaonya,ⁱ nao wakaende-lea kufuata sanamu za uba-tili,^k na wao wenyewe waka-wa ubatili,^l wakiiga mataifa

17:9 *Yaani, kila mahali, penye watu wengi au wachache. **17:10, 16** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **17:12** *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dhara. **17:14** *Tnn., “kufanya shingo zao kuwa ngumu kama shingo za.”

SURA YA 17

a Kut 34:13
Kum 16:21, 22

b Kum 12:2
Isa 57:5

c Law 20:23

d 1Fa 12:28-30
1Fa 21:25, 26

e Kut 20:3-5
Law 26:1
Kum 4:23

f 2Nya 24:18, 19
2Nya 36:15, 16
Yer 25:4

g Isa 55:7

h Kum 1:32
Kum 31:27

i Kum 5:2
Kum 29:12

j Ho 4:6

k Kum 32:21
Isa 12:21

l Zb 115:4-8
Isa 44:9

Safu ya 2

a Kum 12:30

b 1Fa 12:28-30

c 1Fa 14:15
1Fa 16:33

d Kum 4:19
Yer 8:2

e 1Fa 16:30, 31
1Fa 22:51, 53
2Fa 10:21
2Fa 23:4, 5

f 2Fa 16:1, 3

g Kum 18:10
Mik 5:12

h Yos 23:12, 13
Isa 42:24

i 1Fa 14:22
Yer 3:8

j Eze 23:4, 11

k 1Fa 12:20

l 1Fa 12:28-30

yaliyowazunguka pande zote ambayo Yehova alikuwa ame-waamuru wasiyaige.^a

16 Waliendelea kuacha amri zote za Yehova Mungu wao, nao wakatengeneza sanamu za chuma[#] za ndama wawili^b na kutengeneza mti mtakati-fu,^{*c} nao wakaliinamia jeshi lote la mbinguni^d na kumwa-budu Baali.^e **17** Pia waliwate-keteza* motoni wana wao na mabinti wao,^f wakafanya uagu-zi,^{#g} wakatafuta ishara za uba-shiri, na wakaendelea kujitoa[^] wenyewe kutenda maovu ma-choni pa Yehova, na kumkasiri-sha.

18 Kwa hiyo Yehova akawa-kasirikia sana Waisraeli hivi kwamba akawaondoa mbele zake.^h Hakumwacha yeyote abaki isipokuwa watu wa kabila la Yuda peke yao.

19 Hata watu wa kabila la Yuda hawakushika amri za Yehova Mungu wao;ⁱ walifuata pia desturi zilizofuatwa na Waisraeli.^j **20** Yehova aliwa-kataa wazao wote wa Israeli, akawaabisha na kuwatia mikononi mwa waporaji, mpa-ka alipowatupa mbali kutoka mbele zake. **21** Aliwararua Waisraeli kutoka katika nyumba ya Daudi, nao wakamweka Yeroboamu mwana wa Nebati kuwa mfalme.^k Lakini Yeroboamu akasababisha Waisraeli wapotoke na kua-cha kumfuata Yehova, naye akasababisha watende dhambi kubwa. **22** Na Waisraeli wakaendelea kufuata dhambi zote ambazo Yeroboamu alitenda.^l Hawakuziacha

17:16 [#]Tnn., “za kuyeyushwa.” **17:17** [#]Tnn., “waliwagitisha.” [#]Au “wakabashiri.” [^]Tnn., “kujitua.”

23 mpaka Yehova alipowandoa Waisraeli kutoka mbele zake, kama alivyokuwa amesema kupitia watumishi wake wote manabii.^a Kwa hiyo Waisraeli wakaondolewa katika nchi yao na kupelekwa uhamishoni kule Ashuru,^b nao wanaligali huko hadi leo.

24 Kisha mfalme wa Ashuru akawaleta watu kutoka Babiloni, Kutha, Ava, Hamathi, na Sefarvaimu^c na kuwaweka katika majiji ya Samaria ili waishi humo badala ya Waisraeli; nao wakamiliki Samaria na kuishi katika majiji yake. **25** Walipoanza kuishi humo, hawakumwogopa* Yehova. Kwa hiyo Yehova akawatuma simba waje miongoni mwao,^d nao wakawaua baadhi ya watu. **26** Mfalme wa Ashuru akapata habari hii: "Mataifa uliyoyapeleka uhamishoni na kuyaweka katika majiji ya Samaria ili yaishi humo hayajui dini* ya Mungu wa nchi hiyo. Kwa hiyo anaeandelea kuwatuma simba miongoni mwao; na simba hao wanawaua, kwa sababu hakuna yeyote kati yao anayejua dini ya Mungu wa nchi hiyo."

27 Ndiipo mfalme wa Ashuru akaamuru hivi: "Mrudishe ni huko mmoja wa makuhani mliowaleta uhamishoni, aishi huko na kuwafundisha watu hao dini ya Mungu wa nchi hiyo." **28** Basi mmoja wa makuhani ambao walikuwa wamepelekwa uhamishoni kutoka Samaria akarudi na kuishi Betheli,^e naye akaanza kuwafundisha jinsi wanavyopaswa kumwogopa* Yehova.^f

17:25 *Au "hawakumwabudu." 17:26

*Au "hayajui desturi za dini." 17:28

*Au "kumwabudu."

SURA YA 17

a Kum 28:45, 63
1Fa 14:16
Ho 1:4
Amo 5:27
Mik 1:6

b 2Fa 18:11

c 2Fa 19:11, 13

d Kut 23:29

e Mwa 28:18, 19
Yos 16:1
1Fa 12:28, 29

f Yoh 4:20-22

Safu ya 2

a 2Fa 17:24

b 2Fa 18:34

c 1Fa 12:31, 32
1Fa 13:33

d 2Fa 17:24, 41

e Mwa 32:28

f Kut 19:5
Kut 24:7
Kum 29:1

g Kut 20:3-5
Kut 23:24
Kut 34:14
Kum 5:9

29 Hata hivyo, kila taifa likajitengenezea mungu wake na kumweka* katika nyumba za ibada mahali pa juu ambapo Wasamaria walikuwa wamejenga; kila taifa lilifanya hivyo katika majiji walimokuwa wakiishi. **30** Basi wanaume wa Babiloni wakatengeneza Sukoth-benothi, na wanaume wa Kuthi wakatengeneza Nergali, na wanaume wa Hamathi^a wakatengeneza Ashima, **31** na Waavi wakatengeneza Nibhazi na Tartaki. Wasefarvaimu walikuwa wakiwateketeza wana wao motoni kwa ajili ya Adrameleki na Anameleki, miungu ya Sefarvaimu.^b **32** Ingawa walimwogopa Yehova, waliwachagua makuhani kutoka kwa watu wa kawaida ili wahudumu mahali pa juu, na makuhani hao walihudumu kwa niaba yao mahali pa juu katika nyumba za ibada.^c **33** Kwa hiyo walimwogopa Yehova, lakini waliabudu miungu yao wenyewe kulingana na dini* ya mataifa ambamo walitolewa.^d

34 Mpaka leo wanafuata dini* zao za awali. Hakuna yeyote kati yao anayemwabudu[#] Yehova, na hakuna yeyote anayefuata maagizo yake, hukumu zake, na Sheria, na amri ambayo Yehova aliwapa wana wa Yakobo, ambaye alibadili jina lake na kumwita Israeli.^e **35** Yehova alipofanya agano pamoja nao,^f aliwaaamuru hivi: "Msiogope miungu mingine, wala msiinamie wala kuiabudu wala kuitolea dhahibu.^g **36** Lakini mnapaswa kumwogopa Yehova,

17:29 *Au "miungu yake na kuiweka."

17:33, 34 *Au "desturi za dini." 17:34

#Tnn., "anayemwogopa."

aliyewatoa nchini Misri kwa nguvu nyingi na kwa mko-no ulionyoochwaa,^a Yeye ndiye mnayepaswa kumwogopa,^b nanyi mnapaswa kumwinamia yeye, nanyi mnapaswa kumtolea yeye dhabihu. **37** Nanyi mnapaswa sikuzote kufuata kwa uangalifu masharti, maa-muzi, Sheria, na amri aliyowaandikia,^c na hampaswi kuogopa miungu mingine. **38** Na hampaswi kusahau agano nililofanya pamoja nanyi,^d na hampaswi kuogopa miungu mingine. **39** Lakini mnapaswa kumwogopa Yehova Mungu wenu, kwa kuwa yeye ndiye atakayewaokoa kutoka mikononi mwa maadui wenu wote.”

40 Lakini hawakutii, nao wakafuata dini* yao ya awali.^e **41** Kwa hiyo mataifa hayo yakamwogopa Yehova,^f lakini yalikuwa pia yakiabudu sanamu zao za kuchongwa. Wana wao na wajukuu wao wamekuwa wakitenda kama mababu zao mpaka leo hii.

18 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Hoshea^g mwana wa Ela mfalme wa Israeli, Hezekia^h mwana wa Mfalme Ahaziⁱ wa Yuda akawa mfalme. **2** Alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 29 huko Yerusalemu. Mama yake alitwa Abi* binti ya Zekaria.^j **3** Aliendelea kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova,^k kama alivyofanya Daudi babu yake.^l **4** Yeye ndiye aliyeeondoa mahali pa juu,^m akazivunjavunja nguzo takatifu, na kuu-kata ule mti mtakatifu.*ⁿ Pia

17:40 *Au “desturi za dini.” 18:2 *Ufupisho wa jina Abiayi. 18:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 17

- a Kut 6:6
b Kum 6:12, 13
c Kum 31:9
d Kum 4:23
e 2Fa 17:34
f Ezz 4:1, 2

SURA YA 18

- g 2Fa 15:30
2Fa 17:1
h 2Nya 28:27
Mt 1:9
i 2Fa 16:2, 20
j 2Nya 29:1, 2
k 2Fa 20:3
2Nya 31:20, 21
Zb 119:128
l 1Fa 15:5
m Hes 33:52
1Fa 3:2
2Fa 14:1, 4
n Kum 7:5
Kum 12:3
2Nya 31:1

Safu ya 2

- a Hes 21:8, 9
b 2Fa 19:15
2Nya 32:7, 8
c Kum 10:20
Yos 23:8
d 2Fa 16:7
e 2Nya 28:18, 19
Isa 14:28, 29
f 2Fa 17:1
g 2Fa 17:3-6
h Ho 13:16
Amo 3:11
Mik 1:6
i Isa 8:4
Amo 6:1, 7
j 2Fa 17:6
1Nya 5:26

alimpondaponda yule nyoka wa shaba aliyetengenezwa na Musa;^a kwa maana mpaka wakati huo Waisraeli walikuwa wakimfukizia moshi wa dhabihu, na nyoka huyo alikuwa akiitwa sanamu ya nyoka wa shaba.* **5** Alimtumaini Yehova^b Mungu wa Israeli; na hakuna mfalme yeyote kati ya wafalme wote wa Yuda aliyekuwa kama yeye, kabla yake wala baada yake. **6** Alishikamana kabisa na Yehova.^c Hakugeuka na kuacha kumfuata; aliendelea kushika amri ambazo Yehova alimpa Musa. **7** Na Yehova alikuwa pamoja naye. Popote alipoe-nda, alitenda kwa hekima. Alimwasi mfalme wa Ashuru na kukataa kumtumikia.^d **8** Aliwashinda pia Wafilisti^e mpaka Gaza na maeneo yake, kuanzia mnara wa walinzi mpaka jiji lenye ngome.*

9 Katika mwaka wa nne wa utawala wa Mfalme Hezekia, yaani, mwaka wa saba wa Hoshea^f mwana wa Ela mfalme wa Israeli, Mfalme Shalmanesa wa Ashuru alikuja kushambulia Samaria, akaanza kulizingira.^g **10** Nao wakaliteka^h baada ya miaka mitatu; Samaria lilitekwakwa katika mwaka wa sita wa utawala wa Hezekia, ambao ulikuwa mwaka wa tisa wa utawala wa Mfalme Hoshea wa Israeli. **11** Kisha mfalme wa Ashuru akawapeleka Waisraeli uhamishoniⁱ kule Ashuru na kuwaweka katika eneo la Hala na Habori kando ya mto Gozani na katika majiji ya Wamedii ili waishi humo.^j **12** Walipelekwakwa huko

18:4 *Au “akiitwa Nehushtani.” 18:8 *Yaani, kila mahali, penye watu wengi au wachache.

kwa sababu hawakuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wao, badala yake waliendelea kuvunja agano lake, mambo yote ambayo Musa mtumishi wa Yehova aliamuru.^a Hawakusikiliza wala kutii.

13 Katika mwaka wa 14 wa utawala wa Mfalme Hezekia, Senakeribu mfalme wa Ashuru^b alipanda kuja kuyashambulia majiji yote yenye ngome ya Yuda na kuyateka.^c

14 Kwa hiyo Mfalme Hezekia wa Yuda akatuma ujumbe huu kwa mfalme wa Ashuru kule Lakishi: "Nimekosea. Ondokeni, msinishambulie, nami nitalipa chochote mtakachonitoza." Mfalme wa Ashuru akamtoza Mfalme Hezekia wa Yuda faini ya talanta 300 za fedha* na talanta 30 za dhahabu. **15** Basi Hezekia akawapa fedha yote iliyoikuwa katika nyumba ya Yehova na katika hazina za nyumba ya mfalme.*^d **16** Wakati huo Hezekia aling'oa* milango ya hekalu^e la Yehova na miimo ambayo yeye mwenyewe, Mfalme Hezekia wa Yuda, alikuwa ameifunika kwa dhahabu,^f naye akampa mfalme wa Ashuru.

17 Kisha mfalme wa Ashuru akamtuma Tartani,* Rabсарisi,[#] na Rabshake^Δ pamoja na jeshi kubwa kutoka Lakishi^g kwenda kwa Mfalme Hezekia kule Yerusalemu.^h Wakapanda kwenda Yerusalemu na kujipanga karibu na mfereji wa kidi-

18:14 * Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. **18:15** * Au "jumba la." **18:16** * Tnn., "alikata na kuondoa." **18:17** * Au "kamanda." [#] Au "ofisa mkuu wa makao ya mfalme." ^Δ Au "msimamizi mkuu wa vinyaji vya mfalme."

SURA YA 18

a Kum 8:20
1Fa 14:15

b Isa 10:5

c 2Nya 32:1
Isa 36:1

d 2Fa 12:18
2Fa 16:8
2Nya 16:2, 3

e 1Fa 6:33-35

f 2Nya 29:1, 3

g Yos 15:20, 39
2Nya 11:5, 9

h 2Nya 32:9

Safu ya 2

a Isa 36:2, 3

b 2Fa 19:2
Isa 22:20-24

c Isa 22:15-19

d 2Nya 32:10
Isa 36:4-10

e 2Fa 18:7

f Isa 30:1, 2

g 2Nya 32:8

h 2Nya 31:1

i Kum 12:11, 13
2Nya 32:12

j Isa 10:12, 13

mbwi cha juu, kwenye barabara kuu ya uwanja wa mfuaji wa nguo.^a **18** Walipomwita mfalme atoke nje, Eliakimu^b mwana wa Hilikia, aliyekuwa msimamizi wa nyumba,* Shebna^c aliyekuwa mwandishi, na Yoa mwana wa Asafu aliyefanya kazi ya kuweka kumbukumbu, wakaenda nje kukutana nao.

19 Basi Rabshake akawambia: "Tafadhali, mwambieni hivi Hezekia: 'Mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru, anauliza, "Ujasiri wako unategemea msingi gani?"^d **20** Unasema, 'Nina mbinu na nguvu za kupigana vita,' lakini hayo ni maneno matupu. Unamtumaini nani, hivi kwamba unathubutu kuniasi mimi?'^e **21** Tazama! Unautumaini msaada wa utete huu uliopondeka, Misri,^f ambao mtu yeyote akiuegemea utamchoma kiganja na kukitoboa. Hivyo ndivyo Farao mfalme wa Misri alivyo kwa wote wanao mtumaini. **22** Nawe ukiniambia, 'Tunamtumaini Yehova Mungu wetu,'^g je, si yeye ndiye ambaye mahali pake pa juu na madhabahu zake zimeondolewa na Hezekia,^h huku akiwaambia watu wa Yuda na Yerusalemu, 'Mnapaswa kuinama mbele ya madhabahu hii hapa Yerusalemu?'"ⁱ **23** Basi sasa, tafadhali, fanya mkataba huu pamoja na bwana wangu mfalme wa Ashuru: nitakupa farasi 2,000 ikiwa unaweza kupata wapanda farasi wa kutosha idadi hiyo.^j **24** Basi, unawezaje kumzuia hata gavana mmoja aliye mdogo zaidi kati ya watumishi wa bwana wangu, huku ukiitumaini nchi ya Misri ili upate

18:18 * Au "jumba la mfalme."

magari ya vita na wapanda farasi? **25** Sasa je, nimepanda kuja kushambulia mahali hapa ili kupaharibu bila kupewa idhini na Yehova? Yehova mwenyewe aliniambia, 'Panda uende kuishambulia nchi hii na kuiharibu.'"

26 Ndipo Eliakimu mwana wa Hilikia, na Shebna^a na Yoa wakamwambia Rabshake:^b "Tafadhali, zungumza nasi watumishi wako kwa lugha ya Kiaramu,^{*c} kwa maana tuna-weza kuielewa; usizungumze nasi kwa lugha ya Wayahudi huku watu walio ukutani wakisikia."^d **27** Lakini Rabshake akawaambia: "Je, bwana wangu amenituma niwaambie ninyi na bwana wenu tu maneno haya? Je, sipaswi kuwaambia pia wanaume wanaoke-ti ukutani, wale watakaokula kinyesi chao wenyewe na kunywa mkojo wao wenyewe pamoja nanyi?"

28 Kisha Rabshake akasimama na kusema hivi kwa sauti kubwa kwa lugha ya Wayahudi: "Sikieni neno la mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru."^e **29** Mfalme anasema hivi: 'Msikubali Hezekia awadanganye, kwa maana hawezi kuwaokoa kutoka mikononi mwangu.'^f **30** Na msikubali Hezekia awafanye mumtumaini Yehova mkisema: "Kwa hakika Yehova atatuokoa, na jiji hili halitatiwa mikononi mwa mfalme wa Ashuru."^g **31** Msimsikilize Hezekia, kwa maana mfalme wa Ashuru anasema hivi: "Fanyeni amani pamoja nami na mjisalimisha,^{*} na kila

18:26 *Au "Kisiria." **18:31** *Tnn., "Fanyeni baraka pamoja nami na mtoke nje na kuja kwangu."

SURA YA 18

a 2Fa 18:18

b 2Fa 18:17

c Ezz 4:7
Da 2:4

d Isa 36:11, 12

e Isa 36:13-20

f 2Nya 32:15

g 2Fa 19:32-34

Safu ya 2

a 2Fa 17:6

b Hes 13:21

c 2Fa 17:24

d 2Fa 17:6

e 2Fa 19:17-19
2Nya 32:15
Isa 37:23

f Isa 36:21, 22

mmoja wenu atakula matunda ya mzabibu wake mwenyewe na matunda ya mtini wake mwenyewe na kunywa maji kutoka katika tangi lake mwenyewe, **32** mpaka nita-kapokuja na kuwapeleka katika nchi iliyo kama nchi yenu wenyewe,^a nchi yenye nafaka na divai mpya, nchi yenye mikate na mashamba ya mizabibu, nchi yenye mizeituni na asali. Ndipo mtakapoishi, nanyi hamtakufa. Msimsikilize Hezekia, kwa maana anawapotosha kwa kusema, 'Yehova atatuokoa.' **33** Je, kuna mungu yeyote kati ya miungu ya mataifa ambaye amewahi kuiokoa nchi yake kutoka mikononi mwa mfalme wa Ashuru? **34** Iko wapi miungu ya Hamathi^b na Arpadi? Iko wapi miungu ya Sefarvaimu,^c Hena, na Iva? Je, imeokoa Samaria kutoka mikononi mwangu?^d **35** Ni mungu yupi kati ya miungu yote ya nchi mbalimbali ambaye ameokoa nchi yake kutoka mikononi mwangu, hivi kwamba Yehova aokoe Yerusalemu kutoka mikononi mwangu?"^e

36 Lakini watu walikaa kimya, hawakumjibu neno lote, kwa maana mfalme alikuwa amewaagiza hivi: "Msimjibu."^f **37** Lakini Eliakimu mwana wa Hilikia, aliyekuwa msimamizi wa nyumba,^{*} Shebna aliyekuwa mwandishi, na Yoa mwana wa Asafu aliye-kuwa akifanya kazi ya kuweka kumbukumbu wakaja kwa Hezekia mavazi yao yakiwa yameraruliwa, wakamwambia maneno ya Rabshake.

18:37 *Au "jumba la mfalme."

19 Mara tu Mfalme Hezekia aliposikia hilo, akayararua mavazi yake na kuvaa nguo za magunia na kuingia katika nyumba ya Yehova.^a **2** Kisha akamtuma Eliakimu, aliyekuwa msimamizi wa nyumba,* Shebna aliyekuwa mwandishi, na wazee miongoni mwa makuhani, wakiwa wamevaa nguo za magunia, waende kwa nabii Isaya,^b mwana wa Amози. **3** Wakamwambia: "Hezekia anasema hivi: 'Leo ni siku ya taabu, ya kemeo,* na ya aibu; kwa maana watoto wako tayari kuzaliwa,[#] lakini hakuna nguvu za kuwazaa.^c **4** Huenda Yehova Mungu wako atayasikia maneno yote ya Rabshake, aliyetumwa na bwana wake mfalme wa Ashuru ili amdhihaki Mungu aliye hai,^d naye atamfanya awajibike kwa sababu ya maneno ambayo Yehova Mungu wako amesikia. Basi toa sala^e kwa niaba ya watu waliobaki ambao wameokoka.'"

5 Kwa hiyo watumishi wa Mfalme Hezekia wakaenda kwa Isaya,^f **6** naye Isaya akawaambia: "Mwambieni hivi bwana wenu, 'Yehova anasema hivi: "Usiogope^g kwa sababu ya maneno uliyosikia, maneno ambayo watumishi wa mfalme wa Ashuru waliyasema na kunikufuru.^h **7** Sasa ninatia wazo fulani akilini mwake,* naye atasikia habari na kurudi katika nchi yake mwenyewe; nami nitamuua kwa upanga katika nchi yake mwenyewe.'"

19:2 *Au "jumba la mfalme." **19:3** *Au "matusi." [#]Tnn., "wamefika kwenye mlango wa tumbo la uzazi." **19:7** *Tnn., "ninatia roho fulani ndani yake."

SURA YA 19

a Isa 37:1-4

b Isa 1:1

c Isa 26:17, 18

d 1Sa 17:45
2Fa 18:35e 2Sa 22:7
2Nya 20:9
2Nya 32:20
Zb 50:15

f Isa 37:5-7

g Kum 20:3
Isa 41:10
Isa 51:7

h 2Fa 18:17

i 2Nya 32:21
Isa 37:37, 38

Safu ya 2

a 2Fa 18:14

b Isa 37:8-13

c 2Fa 18:17

d 2Nya 32:15

e 2Fa 17:5
2Nya 32:10, 13
Isa 10:8-11

f Mwa 11:31

g 2Fa 17:24
2Fa 18:33, 34h 1Fa 8:30
Isa 37:14-20

i 2Nya 32:20

j Kut 25:22

k 1Nya 29:10, 11

l 1Fa 8:29
Zb 65:2m 2Nya 16:9
Da 9:18

8 Baada ya Rabshake kusi-
kia kwamba mfalme wa Ashu-
ru ameondoka Lakishi,^a aliru-
di na kumkuta akipigana vita
na Libna.^b **9** Ndio mfalme
akasia maneno haya yakise-
mwa kumhusu Tirhaka mfa-
lme wa Ethiopia: "Ametoka ili
kuja kupigana nawe." Kwa
hiyo akawatuma tena waju-
mbe^c kwa Hezekia, akisema:
10 "Mwambieni hivi Mfalme
Hezekia wa Yuda: 'Usikuba-
li Mungu wako unayemtumai-
ni akudanganye akisema: "Ye-
rusalemu halitatiwa mikono-
ni mwa mfalme wa Ashuru."^d
11 Tazama! Umesikia mambo
ambayo wafalme wa Ashuru
walizitendea nchi zote kwa
kuziangamiza.^e Je, ni wewe
peke yako utakayeokolewa?
12 Je, miungu ya mataifa ya-
liyoangamizwa na mababu ya-
ngu iliyaokoa mataifa hayo?
Gozani, Harani,^f Resefu, na
watu wa Edeni waliokuwa Tel-
asari wako wapi? **13** Yuko
wapi mfalme wa Hamathi,
mfalme wa Arpadi, na mfalme
wa majiji ya Sefarvaimu, na
wa Hena, na wa Iva?"^g

14 Hezekia akachukua ba-
rua hizo kutoka mikononi
mwa wajumbe na kuzisoma.
Kisha Hezekia akapanda kwe-
nda katika nyumba ya Yehova,
akazitandaza mbele za Yeho-
va.^h **15** Hezekia akaanza ku-
saliⁱ mbele za Yehova aki-
sema: "Ee Yehova Mungu
wa Israeli, unayeketi kwenye
kiti cha ufalme juu ya* ma-
kerubi,^j wewe peke yako ndi-
ye Mungu wa kweli wa falme
zote za dunia.^k Uliumba mbi-
ngu na dunia. **16** Tega sikio
lako, Ee Yehova, usikie!^l Fu-
ngua macho yako,^m Ee Yehova,

19:15 *Au labda, "katikati ya."

uone! Sikia maneno ambayo Senakeribu amesema ili kudhuhiki wewe Mungu uliye hai. **17** Ee Yehova, ni kweli kwamba wafalme wa Ashuru wameharibu mataifa na nchi zao.^a **18** Nao wameitupa miungu yao motoni, kwa sababu haikuwa miungu^b bali kazi ya mikono ya wanadamu,^c miti na mawe. Ndiyo sababu waliweza kuiangamiza. **19** Lakini sasa, Ee Yehova Mungu wetu, tafadhali tuokoe kutoka mikononi mwake, ili falme zote duniani zijue kwamba wewe peke yako ndiye Mungu, Ee Yehova.”^d

20 Kisha Isaya mwana wa Amози akatuma ujumbe huu kwa Hezekia: “Yehova Mungu wa Israeli anasema, ‘Nimesikia sala yako^e ambayo umenitolea kumhusu Mfalme Senakeribu wa Ashuru.’^f **21** Hili ndilo neno ambalo Yehova amesema dhidi yake:

“Binti bikira wa Sayuni anakudharau, anakudhuhiki.

Binti ya Yerusalemu anakutikisia kichwa.

22 Umemdhuhiki na kumkufuru nani?^g

Umepaza sauti yako dhidi ya nani^h

Na kuinua macho yako yenye kiburi?

Ni dhidi ya Mtakatifu wa Israeli!ⁱ

23 Kupitia wajumbe wako^j umemdhuhiki Yehova^k ukisema,

‘Kwa wingi wa magari yangu ya vita

Nitapanda vilele vya milima,

Sehemu za mbali sana za Lebanoni.

SURA YA 19

a 2Fa 16:8, 9
2Fa 17:6, 24

b Isa 41:29

c Yer 10:3

d Zb 83:17, 18
Isa 45:5, 6

e 2Fa 19:15

f Isa 37:21, 22

g 2Fa 19:10

h 2Fa 18:30
Isa 10:12, 13

i Isa 37:23-25

j 2Fa 18:17

k 2Nya 32:17
Isa 10:10, 11

Safu ya 2

a Isa 14:24

b Zb 33:11

c Isa 46:10

d Isa 10:5
Isa 37:26, 27

e Isa 40:7

f Met 5:21
Ebr 4:13

g Isa 37:28, 29

h Zb 46:6
Isa 10:5, 15

i 2Fa 18:35
Isa 10:12, 13

j Zb 32:9

Nitakata mierezi yake mirefu sana, miberoshi yake iliyo bora.

Nitaingia mahali pake palipo ndani kabisa, misitu yake yenye miti mingi sana.

24 Nitachimba visima na kunywa maji mageni; Nitavikausha vijito vyote vya* Misri kwa nyayo za miguu yangu.’

25 Je, hujasikia? Tangu zamani za kale liliamuliwa.*^a

Tangu siku zilizopita nimeilitayarisha.*^b

Sasa nitalitimiza.^c

Utayabadili majiji yenye ngome yawe marundo ya magofu yenye ukiwa.^d

26 Wakaaji wake hawatakuwa na uwezo;

Wataogopeshwa na kuibishwa.

Watakuwa kama mimea ya shambani na nyasi mbichi,^e

Kama nyasi zilizo kwenye paa zinazokaushwa na upepo wa mashariki.

27 Lakini ninajua vizuri unapoketi, unapotoka nje, unapoingia,^f

Na unapokuwa na ghadhabu dhidi yangu,^g

28 Kwa sababu ghadhabu yako dhidi yangu^h na mngurumo wako umefika masikioni mwangu.ⁱ

Basi nitatia kulabu yangu puani mwako na lijamu yangu^j katikati ya midomo yako,

Nami nitakurudisha kupi-

19:24 *Au “Nitaikausha mifereji yote ya Nile ya.” **19:25** *Tnn., “lilifanywa.”
*Au “nimelitengeza.”

tia njia uliyoitumia kuja.”^a

29 “Na hii ndiyo itakayokuwa ishara kwako: * Mwaka huu utakula mimea inayoota yenyewe; # na katika mwaka wa pili utakula nafaka inayochipuka kutoka katika mimea hiyo; ^b lakini katika mwaka wa tatu utapanda mbegu na kuvuna, nawe utapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake. ^c **30** Watu wa nyumba ya Yuda watakaoponyoka, wale wanaobaki, ^d watatia mizizi chini na kuzaa matunda kwenda juu. **31** Kwa maana waliobaki watatoka Yerusalemu na waokokaji wata-toka katika Mlima Sayuni. Bidii ya Yehova wa majeshi itatenda hayo. ^e

32 “Kwa hiyo Yehova anasema hivi kuhusu mfalme wa Ashuru: ^f

“Hataingia katika jiji hili ^g
Wala hatapiga mshale humo

Wala kulikabili kwa ngao
Wala kujenga boma la kulingira. ^h

33 Atarudi kupitia njia aliyotumia kuja;

Hataingia katika jiji hili,^a
asema Yehova.

34 “Nitalilinda jiji hili na kulio-koa kwa ajili yangu mwenyewe ^j

Na kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu.””^k

35 Usiku huohuo malaika wa Yehova alienda na kuwaua wanaume 185,000 katika kambi ya Waashuru. ^l Watu walipoamka asubuhi na mape-ma, waliona maiti zote hizo. ^m

19:29 * Yaani, Hezekia. # Au “nafaka zilizoanguka na kuota zenyewe.”

SURA YA 19

a 2Fa 19:33

b Law 25:4-6

c Isa 37:30-32

d 2Nya 32:22
Isa 10:20

e Isa 59:17
Zek 1:14, 15

f Isa 10:24

g 2Nya 32:22

h Isa 37:33-35

i Isa 31:5

j 1Sa 12:22
Isa 43:25
Eze 36:22

k 2Fa 20:6
Yer 23:5

l 2Nya 32:21
Isa 31:8

m Kut 12:30
Isa 37:36-38

Safu ya 2

a Yon 1:2

b 2Fa 19:7, 28

c 2Nya 32:21

d Mwa 8:4

e Ezz 4:2

SURA YA 20

f 2Nya 32:24

g Isa 38:1-3

h 2Nya 31:20, 21
Zb 25:7
Zb 119:49

i Isa 38:4-6

j Zb 39:12

k Kum 32:39
Zb 41:3
Zb 103:3
Zb 147:3

l Zb 66:13
Zb 116:12-14

m 2Nya 32:22
Isa 10:24

36 Kwa hiyo Mfalme Senakeribu wa Ashuru akaondo-ka, akarudi Ninawi ^a na kukaa huko. ^b **37** Alipokuwa akiinama chini katika nyumba ya * Nisroki mungu wake, watoto wake mwenyewe wa kiume Adrameleki na Shareza walimuua kwa upanga ^c na kutorokea nchi ya Ararati. ^d Na Esar-hadoni ^e mwanawe akawa mfalme baada yake.

20 Siku hizo Hezekia aka-ka na mgonjwa karibu afe. ^f Nabii Isaya mwana wa Amози akaja na kumwambia, “Yehova anasema hivi: ‘Wape maagizo watu wa nyumba yako, kwa maana utakufa; hutapona.’” ^g **2** Ndipo akaugeza uso wake kuelekea ukutani, akaanza kusali hivi kwa Yehova: **3** “Nakusihii, Ee Yehova, tafadhali, kumbuka jinsi ambavyo nimetembea mbele zako kwa uaminifu na kwa moyo kamili, nami nime-tenda mambo mema macho-ni pako.” ^h Kisha Hezekia akaanza kulia sana na kububujika kwa na machozi.

4 Isaya hakuwa amefika katika ua wa katikati, neno la Yehova lilipomjia likisema: ⁱ **5** “Rudi ukamwambie Hezekia, kiongozi wa watu wangu, ‘Yehova Mungu wa Daudi babu yako anasema hivi: ‘Nimesikia sala yako. Nimeona machozi yako. ^j Tazama, ninakuponya. ^k Siku ya tatu utapanda kwenda katika nyumba ya Yehova. ^l **6** Nitakuongezea miaka 15 ya kuishi, * nami nitakuokoa wewe na jiji hili kutoka mikononi mwa mfalme wa Ashuru, ^m nami nitalilinda jiji

19:37 * Au “hekalu la.” 20:6 * Tnn., “katika siku zako.”

hili kwa ajili yangu mwenyewe na kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu.”^a

7 Ndipo Isaya akasema: “Leteni keki ya tini kavu zilizoshinikizwa.” Basi wakaileta na kuipaka kwenye jipu hilo, kisha akapona hatua kwa hatua.^b

8 Hezekia alikuwa amemuuliza hivi Isaya: “Ni ishara gani^c itakayonionyesha kwamba Yehova ataniponya na kwamba nitapanda kwenda katika nyumba ya Yehova siku ya tatu?”

9 Isaya akajibu: “Hii ndiyo ishara kutoka kwa Yehova itakayokuonyesha kwamba Yehova atatimiza neno alilosema: Je, unataka kivuli kilicho kwenye ngazi* kiende mbele hatua kumi au kirudi nyuma hatua kumi?”^d **10** Hezekia akasema: “Ni rahisi kivuli kwenda mbele hatua kumi lakini si rahisi kirudi nyuma hatua kumi.” **11** Kwa hiyo nabii Isaya akamwomba Yehova, Naye akafanya kivuli kilichokuwa kwenye ngazi ya Ahazi kirudi nyuma hatua kumi na tayari kilikuwa kimeshuka ngazi.^e

12 Wakati huo mfalme wa Babiloni, Berodak-baladani mwana wa Baladani, akamtumia Hezekia barua na zawadi, kwa maana alisikia kwamba Hezekia alikuwa mgonjwa.^f **13** Hezekia akawakaribisha* na kuwaonyesha nyumba yake yote yenye hazina^g—fedha, dhahabu, mafuta ya zeri na mafuta mengine yenye thamani, ghala lake

20:9 *Huenda ngazi hizo zilitumiwa kuonyesha wakati, kama saa ya kivuli inavyoonyesha wakati kwa kufuata mwendo wa jua. **20:13** *Au “akawasiliza.”

SURA YA 20

a 2Fa 19:34
Isa 37:35

b Isa 38:21, 22

c Amu 6:17
Isa 7:11

d Isa 38:7, 8

e Yos 10:12
2Nya 32:31

f Isa 39:1, 2

g 2Nya 32:27

Safu ya 2

a Isa 39:3, 4

b Isa 39:5-7

c 2Fa 24:12, 13
2Fa 25:13
2Nya 36:7, 18
Yer 27:21, 22
Da 1:2

d 2Fa 24:12

e Da 1:19
Da 2:49

f Zb 141:5

g Isa 39:8

la silaha, na kila kitu kilichokuwa katika hazina zake. Hakuna kitu chochote ambacho Hezekia hakuwaonyesha katika nyumba yake mwenyewe* na katika milki yake yote.

14 Kisha nabii Isaya akienda kwa Mfalme Hezekia na kumuuliza: “Watu hawa wali-sema nini, nao walitoka wapi?” Hezekia akajibu: “Walitoka katika nchi ya mbali, kutoka Babiloni.”^a **15** Kisha akauliza: “Waliona nini katika nyumba yako?”^b Hezekia akajibu: “Waliona kila kitu katika nyumba yangu.”^c Hakuna chochote ambacho sikuwaonyesha katika hazina zangu.”

16 Sasa Isaya akamwambia Hezekia: “Sikia neno la Yehova,^b **17** ‘Tazama! Siku zinakuja, na vitu vyote vilivyo katika nyumba yako* na vitu vyote ambavyo mababu zako wamehifadhi mpaka leo hii vitapelekwa Babiloni.^c Hakuna chochote kitakachobaki,’ asema Yehova. **18** ‘Na baadhi ya wana wako mwenyewe utakaowazaa watachukuliwa^d na kuwa maafisa wa makao ya mfalme katika jumba la mfalme wa Babiloni.’”^e

19 Ndipo Hezekia akamwambia Isaya: “Neno la Yehova ambalo umesema ni jema.”^f Kisha akasema: “Ni jema ikiwa kutakuwa na amani na utulivu* wakati wa maisha yangu.”^g

20 Na mambo mengine katika historia ya Hezekia, ukuu wake wote na jinsi alivyote-

20:13 *Au “jumba lake la kifalme.”

20:15 *Au “jumba lako la mfalme?”

^aAu “jumba langu la mfalme.” **20:17**

*Au “jumba lako la mfalme.”

20:19 *Au “ukweli.” ^bTnn., “katika siku zangu.”

ngeneza kile kidimbwi^a na ule mfereji na kuleta maji jijini,^b je, hayajaandikwa katika kitaibu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **21** Kisha Hezekia akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake;^c na Manase mwanawe^d akawa mfalme baada yake.^e

21 Manase^f alikuwa na umri wa miaka 12 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 55 huko Yerusalemu.^g Mama yake alitwa Hefziba. **2** Manase alitenda maovu machoni pa Yehova, akafuata mazoea yenye kuchukiza ya mataifa^h ambayo Yehova alikuwa ameyafukuza kutoka mbele ya Waisraeli.ⁱ **3** Alijenga upya mahali pa juu ambapo Hezekia baba yake alikuwa amebomoa,^j akajenga madhabahu kwa ajili ya Baali na kutengeneza mti mtakatifu,^{*k} kama alivyofanya Ahabu mfalme wa Israeli.^l Naye akaliinamia jeshi lote la mbinguni na kuliabudu.^m **4** Alijenga pia madhabahu katika nyumba ya Yehova,ⁿ ambayo Yehova alikuwa amesema hivi kuihusu: "Nitaweka jina langu Yerusalemu."^o **5** Naye alijenga madhabahu kwa ajili ya jeshi lote la mbinguni^p katika nyua mbili za nyumba ya Yehova.^q **6** Naye alimtekeza* motoni mwana wake mwenyewe; alifanya uchawi, alitafuta ishara za ubashiri,^r na kuwaweka rasmi watu wanaowasiliana na roho na wabashiri.^s Alitenda kwa kiwango kiku-bwa sana mambo maovu machoni pa Yehova, na kumkasi-risha.

21:3, 7 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
21:6 *Tnn., "alimpitisha."

SURA YA 20

a Yoh 9:11

b 2Nya 32:30

c 1Fa 2:10

d 2Fa 21:16
2Fa 23:26
2Nya 33:11-13

e 2Nya 32:33

SURA YA 21

f 1Nya 3:13

Mt 1:10

g 2Nya 33:1

h Kum 12:30, 31

2Nya 36:14

Eze 16:51

i 2Nya 33:2-6

j 2Fa 18:1, 4

k 2Fa 23:4

l 1Fa 16:30, 32

m Kum 4:19

n Yer 32:34

o Kum 12:5

2Sa 7:12, 13

1Fa 8:29

1Fa 9:3

p Eze 8:16

q 1Fa 6:36

1Fa 7:12

r Law 19:26

s Law 20:27

Kum 18:10, 11

Safu ya 2

a 2Fa 23:6

b 2Nya 33:7-9

c 1Nya 17:9

d Kum 28:1

e Kum 7:1

f 2Nya 33:10
2Nya 36:15, 16
Yer 7:25
Mt 23:37

g Mwa 15:16

h Law 18:24, 25

2Fa 23:26

2Fa 24:3

Yer 15:4

i 2Fa 22:16, 17

Mik 3:12

j Yer 19:3

k Isa 28:17

Omb 2:8

7 Akachukua sanamu ya kuchongwa ya mti mtakatifu*^a aliyokuwa ametengeneza na kuiweka ndani ya nyumba ambayo Yehova alikuwa amemwambia hivi Daudi na Sulemani mwanawe kuihusu: "Nitaweka jina langu milele katika nyumba hii na katika jiji la Yerusalemu, ambalo nimelichagua kati ya makabila yote ya Israeli.^b **8** Nami sitaifanya tena miguu ya Waisraeli itangetange kutoka katika nchi niliyowapa mababu zao^c ikiwa watashika kwa uangalifu mambo yote niliyowaamuru,^d Sheria yote ambayo Musa mtumishi wangu aliwaagiza wafuate." **9** Lakini hawakutii, na Manase aliendelea kuwapotosha, akasababisha watende uovu mkubwa zaidi kuliko uliofanywa na mataifa ambayo Yehova alikuwa ameyaangamiza kutoka mbele ya Waisraeli.^e

10 Yehova aliendelea ku-sema hivi kupitia watumishi wake manabii:^f **11** "Manase mfalme wa Yuda amefanya mambo haya yote yenye kuchukiza; ametenda mambo maovu zaidi kuliko Waamori wote^g waliomtangulia,^h naye amesababisha watu wa Yuda watende dhambi kwa sanamu zake zenye kuchukiza.* **12** Kwa hiyo Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: 'Tazama, ninaleta msiba mkubwa sana Yerusalemuⁱ na Yuda hivi kwamba masikio yote mawili ya yeyote atakayesikia habari zake yatawasha.^j **13** Nami nitanyoosha kamba ya kupimia juu ya Yerusalemu,^k kamba

21:11 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno "mavi," nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

iliyotumika kupima Samaria^a na kutumia timazi iliyotumiwa kupima nyumba ya Ahabu,^b nami nitalifuta kabisa Yerusalemu liwe safi kama mtu anavyofuta bakuli liwe safi, akilifuta na kulipindua.^c **14** Nitawaacha watu waliobaki wa urithi wangu^d na kuwatia mikononi mwa maadui wao, nao wataporwa na kuchukuliwa nyara na maadui wao wote,^e **15** kwa sababu walitenda maovu machoni pangu nao waliendelea kunikasirisha tangu siku ambayo mababu zao walitoka Misri mpaka leo hii.”^f

16 Manase pia alimwaga damu nyingi sana isiyo na hatia mpaka alipojaza Yerusalemu damu hiyo kutoka mwisho mmoja hadi mwingine,^g mbali na dhambi yake aliyosababisha Yuda kutenda kwa kufanya maovu machoni pa Yehova. **17** Na mambo mengine katika historia ya Manase na yote aliyofanya na dhambi alizotenda, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **18** Kisha Manase akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika bustani ya nyumba yake, katika bustani ya Uza,^h na Amoni mwanawe akawa mfalme baada yake.

19 Amoniⁱ alikuwa na umri wa miaka 22 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka miwili huko Yerusalemu.^j Mama yake aliitwa Meshulemethi binti ya Haruzi kutoka Yotba. **20** Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, kama alivyofanya Manase baba yake.^k **21** Aliendelea kutembea katika njia zote ambazo baba yake alitembea, akaendelea kuziabu-

SURA YA 21

a 2Fa 17:6
Eze 23:33b 1Fa 21:21
2Fa 10:11

c Yer 25:9

d Kum 32:9
2Fa 17:18e Law 26:25
Kum 28:63f Kum 9:21
Kum 31:29
Amu 2:11, 13g 2Fa 24:3, 4
Yer 2:34
Mt 23:30
Ebr 11:37

h 2Fa 21:23, 26

i Mt 1:10

j 2Nya 33:21

k 2Nya 33:22, 23

Safu ya 2

a 2Fa 21:1, 3

b 2Fa 22:16, 17
Yer 2:13

c 2Nya 33:25

d 2Fa 21:18

e Mt 1:10

SURA YA 22

f 1Fa 13:2
Yer 1:2
Sef 1:1

g 2Nya 34:1, 2

h Yos 15:20, 39

i 1Fa 15:5

j 2Nya 34:8

k 1Nya 6:13

l 2Fa 12:4, 5
2Nya 24:8m 2Fa 12:9
2Nya 34:9

du na kuziinamia sanamu zenye kuchukiza ambazo baba yake aliabudu.^a **22** Kwa hiyo akamwacha Yehova Mungu wa mababu zake, naye hakutembea katika njia ya Yehova.^b **23** Hatimaye watumishi wa Amoni wakapanga njama dhidi yake na kumuua mfalme Amoni ndani ya nyumba yake mwenyewe. **24** Lakini watu wa nchi hiyo wakawaua wale wote waliopanga njama dhidi ya Mfalme Amoni, nao wakamweka Yosia mwanawe kuwa mfalme baada yake.^c **25** Na mambo mengine katika historia ya Amoni, mambo aliyofanya, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda? **26** Kwa hiyo wakamzika katika kaburi lake katika bustani ya Uza,^d na Yosia mwanawe^e akawa mfalme baada yake.

22 Yosia^f alikuwa na umri wa miaka minane alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 31 huko Yerusalemu.^g Mama yake aliitwa Yedida binti ya Adaya kutoka Boskathi.^h **2** Alitenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova na kutembea katika njia zote za Daudi babu yake,ⁱ naye hakugeuka na kwenda kulia au kushoto.

3 Katika mwaka wa 18 wa Mfalme Yosia, mfalme huyo alimtuma mwandishi Shafani, mwana wa Azalia mwana wa Meshulam, kwenye nyumba ya Yehova,^j akisema: **4** “Panda uende kwa kuhani mkuu Hilikia^k umwambie akusanye pesa zote zinazoletwa katika nyumba ya Yehova^l ambazo walinzi wa malango wanakusanya kutoka kwa watu.^m

5 Waagize wawape wale waliowekwa kusimamia kazi katika nyumba ya Yehova, ili nao wawape wafanyakazi walio katika nyumba ya Yehova wanaopaswa kurekebisha sehemu zilizoharibika za* nyumba hiyo,^a 6 yaani, wawape mafundi, wajenzi, na waashi, ambao watazitumia kununua mbaao na mawe yaliyochongwa ili kurekebisha nyumba hiyo.^b 7 Lakini hawapaswi kudaiwa hesabu yoyote ya matumizi ya pesa wanazopewa, kwa sababu ni waaminifu.”^c

8 Baadaye kuhani mkuu Hilikia akamwambia mwandishi Shafani:^d “Nimepata kitabu cha Sheria^e katika nyumba ya Yehova.” Basi Hilikia akampa Shafani kitabu hicho, naye akaanza kukisoma.^f 9 Kisha mwandishi Shafani akaenda kwa mfalme na kumwambia: “Watumishi wako wamekusanya* pesa zilizopatikana katika nyumba hiyo, nao wamewapa wale wanaosimamia kazi katika nyumba ya Yehova.”^g 10 Pia, mwandishi Shafani akamwambia mfalme: “Kuna kitabu^h ambacho kuhani Hilikia amenipa.” Kisha Shafani akaanza kukisoma mbele ya mfalme.

11 Mara tu mfalme aliposikia maneno ya kitabu hicho cha Sheria, akayararua mavazi yake.ⁱ 12 Halafu mfalme akamwagiza hivi kuhani Hilikia, Ahikamu/ mwana wa Shafani, Akbori mwana wa Mikaya, mwandishi Shafani, na Asaya mtumishi wa mfalme: 13 “Nendeni mkatafute ushauri wa Yehova kwa nia-

22:5 *Au “kurekebisha nyufa zilizo katika.” 22:9 *Tnn., “wamemimina.”

SURA YA 22

a 2Fa 12:11, 12
2Nya 34:10

b 2Nya 34:11

c 2Fa 12:15
2Nya 34:12

d 2Fa 22:3

e Kum 31:24-26

f 2Nya 34:14, 15

g 2Nya 34:16-18

h Kum 31:9

i 2Nya 34:19-21
Yoe 2:13

j 2Fa 25:22
Yer 26:24

Safu ya 2

a Kum 4:24
Kum 29:27
Kum 31:17

b Kut 15:20
Amu 4:4
Ne 6:14
Lu 2:36
Mdo 21:8, 9

c 2Nya 34:22-28

d 2Fa 22:8

e Kut 20:3
Kum 32:17
Amu 2:12
Yer 2:11

f Isa 2:8

g Kum 32:22
Isa 33:14
Yer 7:20
Eze 20:48

h 1Fa 21:29
Yak 4:6

ba yangu, kwa niaba ya watu, na kwa niaba ya watu wote wa Yuda kuhusu maneno ya kitabu hiki ambacho kimepatikana; kwa maana ghadhabu ya Yehova iliyowaka dhidi yetu ni kali,^a kwa sababu mababu zetu hawakutii maneno ya kitabu hiki kwa kuyashika mambo yote yaliyoandikwa kutuhusu.”

14 Basi kuhani Hilikia, Ahikamu, Akbori, Shafani, na Asaya wakaenda kwa nabii wa kiki anayelitwa Hulda.^b Alikuwa mke wa Shalumu mwana wa Tikva mwana wa Harhasi, mtunzaji wa chumba cha mavazi, naye alikuwa akiishi katika Wilaya ya Pili ya Yerusalemu; wakazungumza naye huko.^c 15 Hulda akawaambia, “Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Mwambieni hivi mtu aliyewatuma kwangu: 16 “Yehova anasema, ‘Nitaleta msiba mahali hapa na kwa wakaaji wake, maneno yote ya kitabu ambacho mfalme wa Yuda amesoma.^d 17 Kwa sababu wameniacha na wanafukuzia miungu mingine^e moshi wa dhabihu ili kunikasirisha kwa kazi zote za mikono yao,^f ghadhabu yangu itawaka dhidi ya mahali hapa nayo haitazimwa.”^g 18 Lakini mwambieni hivi mfalme wa Yuda aliyewatuma kutafuta ushauri wa Yehova: “Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Kuhusu maneno ambayo umesikia, 19 kwa sababu moyo wako ulikuwa msikivu,* nawe ukajinyenyekeza^h mbele za Yehova uliposikia mambo niliyosema dhidi ya mahali hapa na wakaaji

22:19 *Tnn., “laini.”

wake—kwamba watakuwa kitu cha kutisha na laana—nawe ukayararua mavazi yako^a na kulia mbele zangu, mimi pia nimekusikia, asema Yehova. **20** Ndiyo sababu nitakuzika pamoja na mababu zako,* nawe utalazwa kwa amani katika kaburi lako, na macho yako hayataona msiba wote nitakaoleta mahali hapa.”””” Kisha wakampelekea mfalme jibu hilo.

23 Basi mfalme akatuma ujumbe, na wazee wote wa Yuda na Yerusalemu wakakusanywa.^b **2** Baada ya hayo mfalme akapanda kwenenda katika nyumba ya Yehova pamoja na wanaume wote wa Yuda, wakaaji wote wa Yerusalemu, makuhani, na manabii—watu wote, kuanzia mdogo mpaka mkubwa. Akasoma, watu wote wakisikia, maneno yote ya kitabu^c cha agano^d kilichokuwa kimepatikana katika nyumba ya Yehova.^e **3** Mfalme akasimama karibu na nguzo na kufanya agano* mbele za Yehova,^f kwamba atamfuata Yehova na kushika amri zake, vikumbusho vyake, na sheria zake kwa moyo wake wote na kwa nafsi^g yake yote kwa kutekeleza maneno ya agano hilo yaliyoandikwa katika kitabu hicho. Watu wote wakakubali agano hilo.^g

4 Halafu mfalme akamwagiza kuhani mkuu Hilikia,^h makuhani wa daraja la pili, na walinzi wa milango waondoe kutoka katika hekalu la Yehova vyombo vyote vilivyov-

22:20 *Tnn., “nitakukusanya kwa watu wako.” Huu ni msembo wa kishairi unao-rejelea kifo. **23:3** *Au “kufanya upya lile agano.” **23:3, 4, 6, 7** *Angalia Kamasi, uku. 2012.

SURA YA 22

a 2Fa 22:11

SURA YA 23

b 2Nya 34:29, 30

c Kum 31:26

d Kut 24:8

e 2Fa 22:8

f 2Fa 11:17
2Nya 15:10, 12

g Yos 24:24, 25
2Nya 34:31, 32

h 2Fa 22:4

Safu ya 2

a 2Fa 21:1, 7
2Nya 34:4

b 1Fa 12:28, 29

c 2Fa 21:1, 3
Yer 8:1, 2

d 2Fa 21:1, 7

e Kum 7:25

f 2Nya 34:4

g Law 18:22
Kum 23:17, 18
1Fa 15:11, 12
1Fa 22:46

h Yos 21:17, 19
1Fa 15:22

i Mwa 21:31

tengenezwa kwa ajili ya Baali, kwa ajili ya mti mtakatifu,^{#a} na kwa ajili ya jeshi lote la mbinguni. Kisha akaviteketeza nje ya Yerusalemu kwenye matata ya Kidroni, akapeleka majivu yake Betheli.^b **5** Basi akawaondoa kabisa makuhani wa miungu ya kigeni, waliochaguliwa na wafalme wa Yuda kufukiza moshi wa dhabihu mahali pa juu katika majiji ya Yuda na mae-neo yanayozunguka Yerusalemu, na pia wale waliofukiza moshi wa dhabihu kwa Baali, kwa jua, kwa mwezi, kwa makundi ya nyota za unajimu, na kwa jeshi lote la mbinguni.^c **6** Akauondoa mti mtakatifu^{#d} katika nyumba ya Yehova na kupeleka nje ya Yerusalemu, katika Bonde la Kidroni, akaviteketeza^e katika Bonde la Kidroni, akasaga mpaka ukawa mavumbi na kuyatawanya mavumbi hayo juu ya makaburi ya watu wa kawaida.^f **7** Akabomoa pia nyumba za wanaume makahaba wa hekaluni^g zilizokuwa katika nyumba ya Yehova, mahali ambapo wawake walikuwa wakifuma mahema ya ibada ya mti mtakatifu.[#]

8 Kisha akawaondoa makuhani wote katika majiji ya Yuda, naye akafanya mahali pa juu ambapo makuhani walifukizia moshi wa dhabihu pasifaa kwa ibada, kuanzia Geba^h mpaka Beer-sheba.ⁱ Ali-bomoa pia mahali pa juu palipokuwa kwenye malango yaliyokuwa katika njia ya kuingia kwenye lango la Yoshua mkuu wa jiji, malango yaliyokuwa upande wa kushoto mtu anapuingia katika lango la jiji. **9** Makuhani wa ma-

hali pa juu hawakuhudumu kwenye madhabahu ya Yehova kule Yerusalemu,^a lakini walikula mikate isiyo na chachu pamoja na ndugu zao. **10** Pia alipafanya Tofethi,^b palipokuwa katika Bonde la Wana wa Hinomu^c pasifae kwa ibada, ili mtu yeyote asimteketeze[#] motoni mwana wake au binti yake kwa ajili ya Moleki.^d **11** Pia farasi ambao wafalme wa Yuda walikuwa wamewaweka wakfu* kwa jua aliwazuia wasiingie katika nyumba ya Yehova kupitia chumba[#] cha Nathan-meleki ofisa wa makao ya mfalme, chumba kilichokuwa barazani; naye akayateketeza motoni magari yaliyowekwa wakfu kwa jua.^e **12** Mfalme alibomoa pia madhabahu ambazo wafalme wa Yuda walijenga kwenye paa^f la chumba cha juu cha Ahazi, na pia madhabahu ambazo Manase alijenga katika nyua mbili za nyumba ya Yehova.^g Alizivunjavunja na kutawanya mavumbi yake katika Bonde la Kidroni. **13** Na mahali pa juu palipokuwa mbele ya Yerusalemu upande wa kusini* wa Mlima wa Uharibifu,[#] mahali ambapo Sulemani mfalme wa Israeli alijenga kwa ajili ya Ashtorethi mungu wa kike mwenye kuchukiza wa Wasidoni; kwa ajili ya Kemoshi mungu mwenye kuchukiza wa Moabu; na kwa ajili ya Milkomu^h mungu

23:10 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Gehena." #Tnn., "asimpitishe." **23:11** *Tnn., "wamewatoa." #Au "chumba cha kulia chakula." **23:13** *Tnn., "kulia." Yaani, kusini, mtu anapotazama mashariki. #Yaani, Mlima wa Mizeituni, hasa upande wa kusini ulio mbali zaidi unaojulikana pia kama Mlima wa Kosa.

SURA YA 23

a Eze 44:10
Mal 2:7, 8

b Yer 7:31

c Yos 15:8

d 2Fa 16:2, 3
Yer 32:35

e Kum 4:19
Eze 8:16

f Yer 19:13
Sef 1:4, 5

g 2Fa 21:1, 5

h Sef 1:4, 5

Safu ya 2

a 1Fa 11:5, 7

b Kut 23:24
Kum 7:5
2Nya 34:1, 3

c 1Fa 12:28, 33

d 2Nya 34:6, 7

e 1Fa 13:2

f 1Fa 13:1

g 1Fa 13:30, 31

h 1Fa 12:25, 31
1Fa 13:32
2Fa 17:9

mwenye kuchukiza wa Waa-
moni,^a mfalme alipafanya pasifae kwa ibada. **14** Naye akavunjavunja nguzo takatifu, akaikata miti mitakatifu^{*b} na kujaza mahali pake mifupa ya binadamu. **15** Alibomoa pia madhabahu iliyokuwa Betheli, mahali pa juu ambapo Yeroboamu mwana wa Nebati alijenga na ambapo palisababisha Waisraeli watende dhambi.^c Baada ya kuibomoa madhabahu hiyo na mahali pa juu, aliteketeza mahali hapo pa juu, akapasagasaga pakawa mavumbi, na kuuteketeza mti mtakatifu.^{*d}

16 Yosia alipogeuka na kuona makaburi yaliyokuwa mlimani, aliagiza mifupa itolewe katika makaburi hayo na kuteketezwa kwenye madhabahu, akaifanya madhabahu hiyo isifae kwa ibada, kulingana na neno la Yehova lililokuwa limesemwa na mtu wa Mungu wa kweli aliyetabiri kwamba mambo hayo yangetukia.^e **17** Kisha akauliza: "Lile jiwe la kaburi ninaloona pale ni la nani?" Ndipo watu wa jiji hilo wakamjibu: "Ni kaburi la mtu wa Mungu wa kweli kutoka Yuda^f aliye-tabiri mambo haya uliyoitendea madhabahu ya Betheli." **18** Kwa hiyo akasema: "Acheni apumzike. Mtu yeyote asiiguse mifupa yake." Basi wakaiacha mifupa yake pamoja na mifupa ya yule nabii aliye-toka Samaria.^g

19 Yosia pia aliondoa nyumba zote za ibada zilizokuwa mahali pa juu katika majiji ya Samaria,^h ambazo wafalme wa Israeli walijenga na

23:14, 15 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

kumkasirisha Mungu, akazite-
ndea kama alivyozitendea zile
zilizokuwa Betheli.^a **20** Basi
makuhani wote wa mahali pa
juu waliokuwa mahali hapo
akawatoa dhabihu juu ya
madhabahu hizo, naye akate-
keteza mifupa ya wanadamu
juu yake.^b Kisha akarudi Yeru-
salemu.

21 Kisha mfalme akawaa-
muru hivi watu wote: “Fanyeni
Pasaka^c ya Yehova Mungu
wenu kama ilivyoandikwa ka-
tika kitabu hiki cha agano.”^d

22 Pasaka kama hiyo haiku-
wa imewahi kufanywa tangu
siku ambazo waumuzi waliku-
wa wakiongoza Israeli wala si-
kuzote za wafalme wa Israe-
li na wafalme wa Yuda.^e

23 Lakini katika mwaka wa 18
wa utawala wa Mfalme Yosia,
Pasaka hiyo ya Yehova ilifan-
nywa Yerusalemu.

24 Yosia pia aliwaondoa ka-
bisa watu wote waliowasilia-
na na roho, wabashiri,^f sanamu
za terafimu,^g sanamu zenye
kuchukiza,^h na vitu vyote
vyenye kuchukiza vilivyoku-
wa katika nchi ya Yuda na Ye-
rusalemu, ili atekeleze mane-
no ya Sheria^b yaliyoandikwa
katika kitabu ambacho kuha-
ni Hilikia alipata katika nyu-
mba ya Yehova.ⁱ **25** Kabla ya
Yosia hakukuwa na mfalme
yeyote aliyekuwa kama yeye,
ambaye alimrudia Yehova kwa
moyo wake wote na kwa nafsi
yake yote/ na kwa nguvu zake
zote, kulingana na Sheria yote
ya Musa, na baada yake ha-
kutokea yeyote aliyekuwa
kama yeye.

23:24 *Au “miungu ya familia; sanamu.”
^aHuenda neno la Kiebrania linahusiana
na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonye-
sha dharau.

SURA YA 23

a 2Nya 34:6, 7

b 1Fa 13:2

c 2Nya 35:1

d Kut 12:3-14

e 2Nya 35:18, 19

f Law 19:31
Kum 18:10, 11
2Fa 21:1, 6
Isa 8:19

g Mwa 31:19

h Hes 33:52
Kum 12:2

i 2Fa 22:8

j Kum 4:29

Safu ya 2

a 2Fa 21:11, 12
2Fa 24:3, 4
Yer 15:4b Kum 29:28
2Fa 25:11
Eze 23:33c 2Fa 18:11
2Fa 21:13d Kum 12:5
1Fa 8:29
1Fa 9:3e 1Fa 9:15
2Nya 35:20-25
Zek 12:11

f 2Nya 36:1, 2

g Yer 22:11

h 2Fa 24:18

i 2Fa 21:1, 2
2Fa 21:19-21

j 2Fa 23:29

k Yer 39:5
Yer 52:10

26 Hata hivyo, Yehova ha-
kuacha hasira yake kali iliyo-
waka dhidi ya Yuda kwa saba-
bu ya mambo yote yenye ku-
chukiza ambayo Manase alifan-
ya na kumkasirisha Mungu.^a

27 Yehova akasema: “Nitalio-
ndoa Yuda pia mbele za ma-
cho yangu,^b kama nilivyolio-
ndoa Israeli;^c nami nitalikataa
jiji hili nililochagua, Yerusale-
mu, na nyumba ambayo nili-
sema hivi kuihusu: ‘Jina langu
litaendelea kukaa humo.’”^d

28 Na mambo mengine ka-
tika historia ya Yosia, mambo
yote aliyofanya, je, hayajaa-
ndikwa katika kitabu cha his-
toria ya nyakati za wafal-
me wa Yuda? **29** Katika siku
zake Farao Neko mfalme wa
Misri alikuja kukutana na
mfalme wa Ashuru karibu na
Mto Efrati, kisha Mfalme Yo-
sia akaenda kukabiliana naye;
lakini Neko alipomwona, ali-
mua huko Megido.^e **30** Basi
watumishi wake wakasafirisha
maiti yake katika gari la vita
kutoka Megido, wakamleta Ye-
rusalemu na kumzika katika
kaburi lake. Kisha watu nchi-
ni wakamchukua Yehoahazi
mwana wa Yosia wakamtia ma-
futa na kumweka kuwa mfal-
me baada ya baba yake.^f

31 Yehoahazi^g alikuwa na
umri wa miaka 23 alipoanza
kutawala, naye alitawala kwa
miezi mitatu huko Yerusale-
mu. Mama yake alitwa Ham-
mutali^h binti ya Yeremia
kutoka Libna. **32** Yehoaha-
zi alianza kutenda maovu
machoni pa Yehova, alitenda
mambo yote ambayo maba-
bu zake walitenda.ⁱ **33** Farao
Neko^k alimtia gerezani kule Ri-
bla^k katika nchi ya Hamathi,
ili kumzuia asitawale Yerus-

lemu, kisha akaitoza nchi faini ya talanta 100 za fedha* na talanta moja ya dhahabu.^a **34** Isitoshe, Farao Neko alimweka Eliakimu mwana wa Yosia kuwa mfalme baada ya Yosia baba yake na kubadili jina lake kuwa Yehoyakimu; lakini akamchukua Yehoahazi na kumpeleka Misri,^b ambako alifia hatimaye.^c **35** Yehoyakimu alimpa Farao fedha na dhahabu, lakini alilazimika kuitoza nchi kodi ili ampe Farao fedha alizodai. Alimtoza kila mtu nchini kiasi kilichokadiriwa cha fedha na dhahabu cha kumpa Farao Neko.

36 Yehoyakimu^d alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 11 huko Yerusalemu.^e Mama yake aliitwa Zebida binti ya Pedaya kutoka Ruma. **37** Yehoyakimu aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova,^f alitenda mambo yote ambayo mababu zake walienda.^g

24 Katika siku za utawala wa Yehoyakimu, Mfalme Nebukadnezah^h wa Babiloni alikuja kumshambulia, Yehoyakimu akawa mtumishi wake kwa miaka mitatu. Hata hivyo, alimgeuka na kumwasi. **2** Kisha Yehova akaanza kutuma makundi ya wavamizi ya Wakaldayo,ⁱ Wasiria, Wamoabu, na Waamoni yaende kumshambulia. Aliendelea kutuma makundi hayo yawavamie watu wa Yuda ili kuwaangamiza, kulingana na neno la Yehova^j alilosema kupitia watumishi wake manabii. **3** Haki-ka watu wa Yuda walipatwa na

23:33 * Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 23

a 2Nya 36:3

b 2Nya 36:4, 5

c Yer 22:11, 12

d Yer 1:3
Yer 22:18, 19

e 2Nya 36:5

f Yer 26:21
Yer 36:22-24g 2Nya 28:24, 25
2Nya 33:1, 4

SURA YA 24

h Yer 25:1
Yer 46:2
Da 1:1
Da 3:1
Da 4:33

i Hab 1:6

j Law 26:27, 28
Kum 28:15
2Fa 23:27

Safu ya 2

a Law 26:33
Kum 4:26b 2Fa 21:11
2Fa 23:26c 2Fa 21:16
Yer 2:34
Yer 19:4d Yer 15:1
Omb 3:42

e 2Nya 36:8

f Yer 22:18, 19
Yer 36:30

g Yer 46:2

h Hes 34:2, 5

i Mwa 15:18
1Fa 4:21j Yer 24:1
Yer 37:1

k 2Nya 36:8

l Da 1:1

mambo hayo kwa agizo la Yehova, ili kuwaondoa mbele za macho yake^a kwa sababu ya dhambi zote ambazo Manase alitenda,^b **4** na pia kwa sababu ya damu isiyo na hatia aliyomwaga,^c kwa maana alijaza Yerusalemu damu isiyo na hatia na Yehova hakutaka kumsamehe.^d

5 Na mambo mengine katika historia ya Yehoyakimu, mambo yote aliyotenda, je, hayajaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati za wafalme wa Yuda?^e **6** Kisha Yehoyakimu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake;^f na Yehoyakini mwanawe akawa mfalme baada yake.

7 Mfalme wa Misri hakuto-ka tena kamwe katika nchi yake, kwa maana mfalme wa Babiloni alichukua vitu vyote vilivyokuwa vya mfalme wa Misri,^g kuanzia Korongo* la Misri^h mpaka Mto Efrati.ⁱ

8 Yehoyakini^j alikuwa na umri wa miaka 18 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miezi mitatu huko Yerusalemu.^k Mama yake aliitwa Nehushta binti ya Elnathani wa Yerusalemu. **9** Yehoyakini aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, alitenda mambo yote ambayo baba yake alitenda. **10** Wakati huo watumishi wa Mfalme Nebukadnezah wa Babiloni walipanda kwenda kumshambulia Yerusalemu, wakalizingira jiji hilo.^l **11** Mfalme Nebukadnezah wa Babiloni alikuja wakati watumishi wake walipokuwa wakalizingira jiji hilo.

12 Mfalme Yehoyakini wa Yuda akatoka nje kwenda

24:7 * Angalia Kamusi, uku. 2012.

kukutana na mfalme wa Babiloni,^a akiwa pamoja na mama yake, watumishi wake, wakuu wake, na maofisa wa makao yake;^b na mfalme wa Babiloni akamchukua mateka katika mwaka wa nane wa utawala wake.^c **13** Kisha akachukua hazina zote za nyumba ya Yehova na hazina za nyumba ya mfalme.^{*d} Alivikata vipandevipande vyombo vyote vya dhahabu ambavyo Sulemani mfalme wa Israeli alitengeneza katika hekalu la Yehova.^e Hilo lilitendeka kama Yehova alivyokuwa ametabiri. **14** Akawapeleka uhamishoni watu wote wa Yerusalemu, wakuu wote,^f mashujaa wote hodari, na kila fundi na mfua chuma^{*g}—aliwapeleka uhamishoni watu 10,000. Hakuna yeyote aliyebaki isipokuwa watu maskini kabisa nchini.^h **15** Basi akampeleka Yehoyakiniⁱ uhamishoni Babiloni; alimpeleka pia mama ya mfalme, wake za mfalme, maofisa wa makao yake, na viongozi wa nchi, akawapeleka uhamishoni Babiloni kutoka Yerusalemu. **16** Pia mfalme wa Babiloni aliwapeleka uhamishoni Babiloni mashujaa wote, 7,000, na vilevile mafundi na wahunzi* 1,000, wote walikuwa wanaume mashujaa waliozoezwa kupigana vita. **17** Mfalme wa Babiloni alimweka Matania, mjomba wa Yehoyakini,^k kuwa mfalme baada yake na kubadili jina lake kuwa Sedekia.^l

18 Sedekia alikuwa na umri wa miaka 21 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa mia-

24:13 *Au "jumba la mfalme." **24:14** *Au labda, "mjenzi wa maboma ya ulinzi." **24:16** *Au labda, "wajenzi wa maboma ya ulinzi."

SURA YA 24

a 2Nya 36:9,10

Yer 24:1

Eze 17:12

b Yer 29:1, 2

c Yer 52:28

d 2Fa 20:13, 17

e 1Fa 7:48-50

Ezr 1:7

Da 5:2

f Da 1:3, 6

g Yer 24:1

h 2Fa 25:12

i 2Fa 25:27

1Nya 3:17

j Yer 22:24, 25

k 1Nya 3:15

l 2Nya 36:10-12

Yer 37:1

Yer 52:1

Safu ya 2

a 2Fa 23:31

b 2Fa 23:36, 37

Yer 24:8

Yer 37:1, 2

Yer 38:5, 6

Eze 21:25

c 2Fa 23:27

d 2Nya 36:11, 13

Yer 27:12

Yer 38:17

Eze 17:12-15

SURA YA 25

e Yer 27:8

Yer 43:10

Da 4:1

f 2Nya 36:17

Yer 34:2

Eze 24:1, 2

g Isa 29:3

Yer 32:2, 28

Yer 39:1

Yer 52:4, 5

Eze 4:1, 2

Eze 21:21, 22

h Law 26:26

Kum 28:53

Yer 37:21

Yer 38:2

Omb 4:4

Eze 4:16

Eze 5:10, 12

i Yer 52:6-11

j Yer 21:4

Yer 39:2, 4, 7

Eze 33:21

k Eze 12:12

l Yer 21:7

ka 11 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Hamutali^a binti ya Yeremia kutoka Libna.

19 Sedekia aliendelea kute nda maovu machoni pa Yehova, alitenda mambo yote ambayo Yehoyakimu alitenda.^b

20 Mambo hayo yalitukia Yerusalemu na Yuda kwa sababu ya hasira ya Yehova, mpaka alipowatupa mbali kutoka mbele zake.^c Na Sedekia akamwasi mfalme wa Babiloni.^d

25 Katika mwaka wa tisa wa utawala wa Sedekia, katika mwezi wa kumi, siku ya kumi ya mwezi huo, Mfalme Nebukadneza^e wa Babiloni alikuja na jeshi lake lote ku shambulia Yerusalemu.^f Akapiga kambi na kujenga ukuta kulizingira jiji hilo pande zote,^g **2** naye akalizingira jiji hilo mpaka mwaka wa 11 wa utawala wa Mfalme Sedekia.

3 Katika siku ya tisa ya mwezi wa nne njaa ilikuwa kali sana^h jijini, na watu waliokuwemo hawakuwa na chakula.ⁱ

4 Sehemu ya ukuta wa jiji ilibomolewa,^j na wanajeshi wote wakakimbia wakati wa usiku kupitia lango lililokuwa kati ya kuta mbili karibu na bustani ya mfalme, wakati Wakaldayo walipokuwa wakilizingira jiji; naye mfalme akafuata njia inayoelekea Araba.^k

5 Lakini jeshi la Wakaldayo likamfuatia mfalme, nalo likamfikia katika jangwa tambare la Yeriko na wanajeshi wake wote wakatawanyika na kumwacha. **6** Kisha wakamkamata mfalme^l na kumpeleka mpaka kwa mfalme wa Babiloni kule Ribla, nao wakamhukumu. **7** Wakawachinja wana wa Sedekia huku akitazama; kisha Nebukadne-

za akampofusha macho Sedekia, akamfungua kwa pingu za shaba, na kumpeleka Babiloni.^a

8 Katika mwezi wa tano, siku ya saba ya mwezi huo, yaani, mwaka wa 19 wa utawala wa Mfalme Nebukadnezar wa Babiloni, Nebuzaradani^b mkuu wa walinzi, mtumishi wa mfalme wa Babiloni, alikuja Yerusalemu.^c **9** Akateketeza kabisa nyumba ya Yehova,^d nyumba ya mfalme,^e na nyumba zote Yerusalemu;^f aliteketeza pia nyumba ya kila mtu maarufu.^g **10** Na jeshi lote la Wakaldayo lililokuwa pamoja na mkuu wa walinzi lilibomoa kuta zilizozunguka Yerusalemu.^h **11** Nebuzaradani mkuu wa walinzi aliwapeleka uhamishoni watu wote waliobaki jijini, watu waliojilisalimisha kwa mfalme wa Babiloni, na watu wengine.ⁱ **12** Lakini mkuu wa walinzi aliwaacha baadhi ya watu maskini kabisa nchini ili watunze mashamba ya mizabibu na kufanya kazi za kulazimishwa.^j **13** Pia Wakaldayo walivunja vipandevipande nguzo za shaba^k za nyumba ya Yehova na magari^l na Bahari ya shaba,^m vitu vilivyokuwa katika nyumba ya Yehova, nao wakaipoleka shaba hiyo Babiloni.ⁿ **14** Walichukua pia ndoo za kuondolea majivu, sepetu, mikasi ya kukatia tamba za taa, vikombe, na vyombo vyote vya shaba vilivyotumiwa katika utumishi wa hekaluni. **15** Mkuu wa walinzi alichukua vyetezo na mabakuli yaliyotengenezwa kwa dhahabu^o na fedha halisi.^p **16** Shaba yote iliyotumiwa kutengene-

25:9 *Au "jumba la mfalme."

SURA YA 25

a Yer 32:4, 5
Eze 12:12, 13
Eze 17:16

b Yer 40:1

c Yer 52:12-14
Omb 4:12

d 1Fa 9:8
Zb 74:3
Zb 79:1
Isa 64:11
Yer 7:14
Omb 1:10
Omb 2:7
Mik 3:12

e 1Fa 7:1

f Yer 34:22

g 2Nya 36:19

h Ne 1:3
Yer 39:8

i Yer 15:2
Yer 39:9
Yer 52:15, 30
Eze 5:2

j Yer 39:10
Yer 52:16

k 1Fa 7:15

l 1Fa 7:27

m 1Fa 7:23
n 2Fa 20:17
Yer 52:17-20

o 1Fa 7:48, 50

p 2Nya 24:14
2Nya 36:18
Ezr 1:7, 10, 11
Da 5:2

Safu ya 2

a 1Fa 7:47

b 1Fa 7:15

c 1Fa 7:16, 20
Yer 52:21-23

d Ezr 7:1

e Yer 21:1, 2
Yer 29:25, 29

f Yer 52:24-27

g 2Fa 25:8
Yer 39:9
Yer 40:1

h Yer 39:5

i Hes 34:2, 8
1Fa 8:65

j Kum 28:36, 64
2Fa 23:27
Yer 25:11

k Yer 39:13, 14

l Yer 26:24

m 2Fa 22:8

n Yer 40:5, 6

za zile nguzo mbili, ile Bahari, na yale magari ambayo Sulemani alitengeneza kwa ajili ya nyumba ya Yehova, haingeweza kupimwa uzito.^a **17** Kila nguzo ilikuwa na urefu wa mikono 18,^{*b} na kifuniko chake kilikuwa cha shaba; na urefu wa kifuniko hicho ulikuwa mikono mitatu, na wavu pamoja na makomamanga yote yaliyozunguka kifuniko yalitengenezwa kwa shaba.^c Nguzo ya pili pamoja na wavu wake ilifanana na ya kwanza.

18 Mkuu wa walinzi alimchukua pia kuhani mkuu Seraya,^d Sefania^e kuhani wa pili, na walinzi watatu wa milango.^f **19** Pia alimchukua kutoka jijini ofisa mmoja wa makao ya mfalme aliyekuwa msimamizi wa wanajeshi, watu watano waliopatikana jijini walioshirikiana kwa ukaribu na mfalme, na pia mwandishi wa mkuu wa jeshi, aliyewaandikisha watu jeshini, na wanaume 60 kutoka miongoni mwa watu wa kawaida waliokuwa bado jijini. **20** Nebuzaradani^g mkuu wa walinzi aliwachukua na kuwapeleka kwa mfalme wa Babiloni kule Ribla.^h **21** Mfalme wa Babiloni aliwaua na kuwaangamiza huko Ribla katika nchi ya Hamathi.ⁱ Hivyo watu wa Yuda wakaenda uhamishoni kutoka katika nchi yao.^j

22 Mfalme Nebukadnezar wa Babiloni akamchagua Gedalia^k mwana wa Ahikamu^l mwana wa Shafani^m awasimamie watu aliowaacha katika nchi ya Yuda.ⁿ **23** Wakuu wote wa jeshi na wanajeshi wao waliposikia kwamba mfalme wa

25:17 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyoengeza B14.

Babiloni amemchagua Gedalia, mara moja wakaenda kwa Gedalia huko Mispa. Wakuu hao ni Ishmaeli mwana wa Nethania, Yohanani mwana wa Karea, Seraya mwana wa Tanhumethi Mnetofa, na Yaazania mwana wa Mmaakathi, pamoja na wanajeshi wao.^a **24** Gedalia akawaapia hivi pamoja na wanajeshi wao: “Msiogope kuwa watumishi wa Wakaldayo. Kaeni katika nchi hii na kumtumikia mfalme wa Babiloni, na mambo yatawaendea vyema.”^b

25 Na katika mwezi wa saba, Ishmaeli^c mwana wa Nethania mwana wa Elishama, aliyekuwa wa uzao wa kifalme,* akaja na wanaume wengine kumi, nao wakampiga na kumuua Gedalia pamoja na Wayahudi na Wakaldayo waliokuwa pamoja naye huko Mispa.^d **26** Kisha watu wote,

25:25 *Tnn., “mbegu ya ufalme.”

SURA YA 25

a Yer 40:7-9

b Yer 27:12

c Yer 40:15

d Yer 41:1, 2

Safu ya 2

a Yer 42:14

Yer 43:4, 7

b Yer 41:17, 18

c 2Fa 24:8, 12

Yer 24:1

Mt 1:11

d Yer 52:31-34

kuanzia mdogo mpaka mkubwa, pamoja na wakuu wa jeshi, wakaondoka na kwenda Misri,^a kwa sababu waliwagopoa Wakaldayo.^b

27 Na katika mwaka wa 37 tangu Mfalme Yehoyakini^c wa Yuda alipopelekwa uhamishoni, katika mwezi wa 12, siku ya 27 ya mwezi huo, Mfalme Evil-merodaki wa Babiloni, katika mwaka alioanza kutawala, alimwachilia huru Mfalme Yehoyakini wa Yuda kutoka gerezani.^d **28** Alizungumza naye kwa fadhili na kukikweza kiti chake cha ufalme juu zaidi kuliko viti vya wafalme wengine waliokuwa pamoja naye Babiloni. **29** Basi Yehoyakini akavua mavazi yake ya gerezani, na sikuzote za maisha yake alikuwa akila kwenye meza ya mfalme. **30** Naye alipewa chakula kwa ukawaida kutokea kwa mfalme, siku baada ya siku, siku zote za maisha yake.

KITABU CHA KWANZA CHA

MAMBO YA NYAKATI

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Kuanzia Adamu mpaka Abrahamu (1-27)
Wazao wa Abrahamu (28-37)
Waedomu na wafalme wao na mashehe wao (38-54)</p> <p>2 Wana 12 wa Israeli (1, 2)
Wazao wa Yuda (3-55)</p> <p>3 Wazao wa Daudi (1-9)
Uzao wa kifalme wa Daudi (10-24)</p> <p>4 Wazao wengine wa Yuda (1-23)
Yabesi na sala yake (9, 10)
Wazao wa Simeoni (24-43)</p> | <p>5 Wazao wa Rubeni (1-10)
Wazao wa Gadi (11-17)
Wahagri washindwa (18-22)
Nusu ya kabila la Manase (23-26)</p> <p>6 Wazao wa Lawi (1-30)
Waimbaji wa hekaluni (31-47)
Wazao wa Haruni (48-53)
Makao ya Walawi (54-81)</p> <p>7 Wazao wa Isakari (1-5), wa Benjamini (6-12), wa Naftali (13), wa Manase (14-19), wa Efraimu (20-29), na wa Asheri (30-40)</p> |
|--|--|

- 8 Wazao wa Benjamini (1-40)
Wazao wa Sauli (33-40)
- 9 Koo zilizoandikishwa baada ya kurudi kutoka uhamishoni (1-34)
Orodha ya wazao wa Sauli yarudiwa (35-44)
- 10 Kifo cha Sauli na wanawe (1-14)
- 11 Daudi atiwa mafuta na Waisraeli wote kuwa mfalme (1-3)
Daudi ateka jiji la Sayuni (4-9)
Mashujaa hodari wa Daudi (10-47)
- 12 Waliounga mkono utawala wa Daudi (1-40)
- 13 Sanduku la agano laletwa kutoka Kiriath-yearimu (1-14)
Uza auawa (9, 10)
- 14 Daudi aimarishwa kuwa mfalme (1, 2)
Familia ya Daudi (3-7)
Wafilisti washindwa (8-17)
- 15 Walawi wabeba sanduku la agano na kulipeleka Yerusalemu (1-29)
Mikali amdharau Daudi (29)
- 16 Sanduku la agano lawekwa hemani (1-6)
Wimbo wa shukrani wa Daudi (7-36)
“Yehova amekuwa Mfalme!” (31)
Utumishi mbele ya sanduku la agano (37-43)
- 17 Daudi hatajenga hekalu (1-6)
Agano pamoja na Daudi kwa ajili ya ufalme (7-15)
Sala ya Daudi ya shukrani (16-27)
- 18 Ushindi mbalimbali wa Daudi (1-13)
Wasimamizi wa Daudi (14-17)
- 19 Waamoni wawatendea vibaya wajumbe wa Daudi (1-5)
- Daudi awashinda Waamoni na Wasiria (6-19)
- 20 Jiji la Raba latekwa (1-3)
Majitu ya Wafilisti yauawa (4-8)
- 21 Daudi awahesabu watu bila idhini (1-6)
Yehova awaadhibu (7-17)
Daudi ajenga madhabahu (18-30)
- 22 Daudi afanya matayarisho ya kujenga hekalu (1-5)
Daudi ampa Sulemani maagizo (6-16)
Wakuu waamriwa wamsaidie Sulemani (17-19)
- 23 Daudi awapanga Walawi (1-32)
Haruni na wanawe watengwa kando (13)
- 24 Daudi awapanga makuhani katika vikundi 24 (1-19)
Kazi nyingine za Walawi (20-31)
- 25 Wanamuziki na waimbaji wa nyumba ya Mungu (1-31)
- 26 Vikundi vya walinzi wa malango (1-19)
Waweka hazina na maofisa wengine (20-32)
- 27 Maofisa waliomtumikia mfalme (1-34)
- 28 Hotuba ya Daudi kuhusu ujenzi wa hekalu (1-8)
Maagizo aliyompa Sulemani; ampa ramani ya ujenzi (9-21)
- 29 Michango kwa ajili ya hekalu (1-9)
Sala ya Daudi (10-19)
Watu washangilia; utawala wa Sulemani (20-25)
Kifo cha Daudi (26-30)

- 1** Adamu,
Sethi,^a
Enoshi,
2 Kenani,
Mahalaleli,^b
Yaredi,^c
3 Enoko,^d
Methusela,
Lameki,^e

SURA YA 1

- a Mwa 4:25
b Mwa 5:12, 15
c Mwa 5:18
d Ebr 11:5
e Mwa 5:25, 28

Safu ya 2

- a Mwa 5:29
b Mwa 11:10
c Mwa 6:10
d Isa 66:19
e Eze 27:13
f Mwa 10:2
g Mwa 10:3
Eze 27:14

- 4** Noa,^a
Shemu,^b Hamu, na
Yafethi.^c

5 Wana wa Yafethi walikuwa Gomeri, Magogu, Madai, Yavani, Tubali,^d Mesheki,^e na Tirasi.^f

6 Wana wa Gomeri walikuwa Ashkenazi, Rifathi, na Togarma.^g

7 Wana wa Yavani walikuwa Elisha, Tarshishi, Kitimu, na Rodanimu.

8 Wana wa Hamu walikuwa Kushi,^a Misraimu, Putu, na Kanaani.^b

9 Wana wa Kushi walikuwa Seba,^c Havila, Sabta, Raama,^d na Sabteka.

Wana wa Raama walikuwa Sheba na Dedani.^e

10 Kushi akamzaa Nimrodi.^f Nimrodi alikuwa shujaa wa kwanza duniani.

11 Misraimu akamzaa Ludimu,^g Anamimu, Lehabimu, Naftuhimu,^h 12 Pathrusimu,ⁱ Kasluhimu (hao ndio waliowazaa Wafilisti),^j na Katorimu.^k

13 Kanaani akamzaa Sironi,^l mzaliwa wake wa kwanza, na Hethi,^m 14 na pia Wayebusi,ⁿ Waamori,^o Wargigashi,^p 15 Wahivi,^q Waarwia, Wasini, 16 Waarvadi,^r Wasemari, na Wahamathi.

17 Wana wa Shemu walikuwa Elamu,^s Asihuru,^t Arpakshadi, Ludi, na Aramu, na* Usi, Huli, Getheri, na Mashi.^u

18 Arpakshadi akamzaa Shela,^v naye Shela akamzaa Eberi.

19 Eberi alizaa wana wawili. Mmoja aliiitwa Pelegi,^{*w} kwa sababu katika siku zake dunia ilikuwa imegawanyika.[#] Ndugu yake aliiitwa Yoktani.

20 Yoktani akamzaa Almoadadi, Shelefu, Hazarmavethi, Yera,^x 21 Hadoramu, Uzali, Dikla, 22 Obali, Abimae-

1:17 *Wafuatao ni wana wa Aramu. Angalia Mwa 10:23. 1:19 *Maana yake "Mgawanyiko." #Au "wakaaji wa dunia walikuwa wamegawanyika."

SURA YA 1

a Isa 11:11
b Mwa 10:6
c Zb 27:10
d Eze 27:22
e Mwa 10:7
f Mwa 10:8, 9
g Yer 46:9
h Mwa 10:13, 14
i Eze 29:14
j Yos 13:2, 3
k Kum 2:23
Amo 9:7
l Isa 23:2
m Mwa 10:15-18
n Amu 1:21
o Mwa 15:16
Hes 13:29
Kum 3:8
p Kum 7:1
q Yos 9:3, 7
r Eze 27:11
s Eze 4:9
t Eze 27:23
u Mwa 10:22, 23
v Mwa 11:14
w Mwa 11:19
x Mwa 10:26-29

Safu ya 2

a 1Fa 9:28
b Mwa 2:11
Mwa 25:18
c Mwa 11:19
d Mwa 11:21
e Mwa 11:23
f Mwa 11:25
g Mwa 11:26
h Mwa 17:5
i Mwa 21:3
j Mwa 16:11, 12
k Mwa 28:9
l Eze 27:21
m Mwa 25:13-15
n Mwa 25:1-4
o Mwa 37:28
p Ayu 2:11
q Isa 21:13
r Isa 60:6
s Mdo 7:8
t Mwa 25:25
u Mwa 32:28
v Mwa 36:4, 5
w Oba 9

li, Sheba, 23 Ofiri,^a Havila,^b na Yobabu; wote hao walikuwa wana wa Yoktani.

24 Wazao wa Shemu walikuwa

Arpakshadi,
Shela,

25 Eberi,
Pelegi,^c
Reu,^d

26 Serugi,^e
Nahori,^f
Tera,^g

27 Abram, yaani, Abrahamu.^h

28 Wana wa Abrahamu walikuwa Isakaⁱ na Ishmaeli.^j

29 Hizi ndizo asili za koo zao: mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli alikuwa Nebayothi,^k kisha Kedari,^l Adbeeli, Mibsamu,^m 30 Mishma, Duma, Masa, Hadadi, Tema, 31 Yeturi, Nafishi, na Kedema. Hao ndio waliokuwa wana wa Ishmaeli.

32 Wana waliozaliwa na Keturu,ⁿ suria wa Abrahamu, walikuwa Zimrani, Yokshani, Medani, Midiani,^o Ishbaki, na Shua.^p

Wana wa Yokshani walikuwa Sheba na Dedani.^q

33 Wana wa Midiani walikuwa Efa,^r Eferi, Hanoki, Abida, na Eldaa.

Hao wote walikuwa wana wa Keturu.

34 Abrahamu akamzaa Isaka.^s Wana wa Isaka walikuwa Esau^t na Israeli.^u

35 Wana wa Esau walikuwa Elifazi, Reueli, Yeushi, Yalamu, na Kora.^v

36 Wana wa Elifazi walikuwa Temani,^w Omari, Sefo,

Gatamu, Kenasi, Timna, na Amaleki.^a

37 Wana wa Reueli walikuwa Nahathi, Zera, Shamma, na Miza.^b

38 Wana wa Seiri^c walikuwa Lotani, Shobali, Sibeoni, Ana, Dishoni, Ezeri, na Dishani.^d

39 Wana wa Lotani walikuwa Hori na Homamu. Dada ya Lotani alikuwa Timna.^e

40 Wana wa Shobali walikuwa Alvani, Manahathi, Ebal, Shefo, na Onamu.

Wana wa Sibeoni walikuwa Aya na Ana.^f

41 Mwana* wa Ana alikuwa Dishoni.

Wana wa Dishoni walikuwa Hemdani, Eshbani, Ithrani, na Kerani.^g

42 Wana wa Ezeri^h walikuwa Bilhani, Zaavani, na Akani.

Wana wa Dishani walikuwa Usi na Arani.ⁱ

43 Hawa ndio wafalme waliotawala katika nchi ya Edomu/ kabla mfalme yeyote hawajatawala Waisraeli.*^k Bela mwana wa Beori; jiji lake liliitwa Dinhaba. **44** Bela alipokufa, Yobabu mwana wa Zera kutoka Bosra^l alianza kutawala baada yake. **45** Yobabu alipokufa, Hushamu kutoka katika nchi ya Watemani alianza kutawala baada yake. **46** Hushamu alipokufa, Hadadi mwana wa Bedadi, aliyewashinda Wamidiani katika eneo* la Moabu, alianza kutawala baada yake. Jiji lake liliitwa Avithi. **47** Hadadi alipokufa, Samla kutoka Masreka alianza kutawa-

1:41 *Tnn., "Wana." 1:43 *Tnn., "wana wa Israeli." 1:46 *Tnn., "shamba."

SURA YA 1

a Mwa 36:11, 12

b Mwa 36:13

c Mwa 36:8

d Mwa 36:20, 21

e Mwa 36:22

f Mwa 36:23, 24

g Mwa 36:25, 26

h 1Nya 1:38

i Mwa 36:27, 28

j Mwa 32:3

k Mwa 36:31-39

l Yer 49:13

Safu ya 2

a Mwa 36:40-43

SURA YA 2

b Mwa 32:28

c Mwa 29:32
Mwa 49:3, 4

d Mwa 29:33

e Mwa 29:34
Mwa 49:5-7f Mwa 29:35
Mwa 49:8-12
Ebr 7:14g Mwa 30:18
Mwa 49:14, 15h Mwa 30:20
Mwa 49:13i Mwa 30:4-6
Mwa 49:16-18j Mwa 30:22, 24
Mwa 49:22-26k Mwa 35:16, 18
Mwa 49:27l Mwa 30:7, 8
Mwa 49:21m Mwa 30:9-11
Mwa 49:19n Mwa 30:12, 13
Mwa 49:20

o Mwa 38:2-5

p Mwa 38:7

q Mwa 38:11

r Lu 3:23, 33

s Hes 26:21

la baada yake. **48** Samla alipokufa, Shauli kutoka Rehobothi karibu na ule Mto alianza kutawala baada yake. **49** Shauli alipokufa, Baalhanani mwana wa Akbori alianza kutawala baada yake. **50** Baalhanani alipokufa, Hadadi alianza kutawala baada yake. Jiji lake liliitwa Pau, na mke wake alitwa Meheta-beli binti ya Matredi, binti ya Mezahabu. **51** Kisha Hadadi akafa.

Mashehe* wa Edomu walikuwa Shehe Timna, Shehe Alva, Shehe Yethethi,^a **52** Shehe Oholibama, Shehe Ela, Shehe Pinoni, **53** Shehe Kenasi, Shehe Temani, Shehe Mib-sari, **54** Shehe Magdieli, na Shehe Iramu. Hao ndio waliokuwa mashehe wa Edomu.

2 Hawa ndio waliokuwa wana wa Israeli:^b Rubeni,^c Simeoni,^d Lawi,^e Yuda,^f Isakari,^g Zabuloni,^h **2** Dani,ⁱ Yosefu,^j Benjamin,^k Naftali,^l Gadi,^m na Asheri.ⁿ

3 Wana wa Yuda walikuwa Eri, Onani, na Shela. Binti ya Shua, mwanamke Mkanani, alimzalia wana hao wata-tu.^o Lakini Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, hakumpe-ndeza Yehova, kwa hiyo Akamuua.^p **4** Tamari,^q binti mkwe wa Yuda, alimzalia Yuda wana waliotwa Perezir^r na Zera. Yuda alikuwa na jumla ya wana watano.

5 Wana wa Perezir walikuwa Hezroni na Hamuli.^s

6 Wana wa Zera walikuwa Zimri, Ethani, Hemani, Kal-koli, na Dara. Wote walikuwa watano.

1:51 *Shehe alikuwa mkuu wa kabila.

7 Mwana* wa Karmi alikuwa Akari,[#] aliyewaletea Waisraeli msiba,^{Δa} ambaye alikosa uaminifu kuhusiana na kitu kilichopaswa kuhari-biwa.^b

8 Mwana* wa Ethani alikuwa Azaria.

9 Wana waliozaliwa na Hezroni walikuwa Yerahmeeli,^c Ramu,^d na Kelubai.*

10 Ramu alimzaa Aminadabu.^e Aminadabu akamzaa Nashoni^f mkuu wa wazao wa Yuda. 11 Nashoni akamzaa Salma.^g Salma akamzaa Boazi.^h 12 Boazi akamzaa Obedi. Obedi akamzaa Yese.ⁱ 13 Yese akamzaa mzaliwa wake wa kwanza Eliabu, wa pili Abinadabu,^j wa tatu Shimea,^k 14 wa nne Nethaneli, wa tano Radai, 15 wa sita Ozemu, na wa saba Daudi.^l 16 Dada zao walikuwa Seruya na Abigaili.^m Wana wa Seruya walikuwa Abishai,ⁿ Yoabu,^o na Asaheli,^p wana watatu. 17 Abigaili alimzaa Amasa,^q na baba ya Amasa alikuwa Yetheri, Mwishmaeli.

18 Kalebu* mwana wa Hezroni aliwazaa wana kupitia Azuba mke wake na kupitia Yeriothi; na hawa ndio waliokuwa wana wa Azuba: Yesheri, Shobabu, na Ardoni. 19 Azuba alipokufa, Kalebu alimwoa Efrathi,^r aliyemza-

2:7, 8, 31 *Tnn., "Wana." 2:7 #Maana yake "Mleta Msiba; Anayesababisha Watu Watengwe." Katika Yos 7:1, anaitwa pia Akani. ^ΔAu "taabu; aliyesababisha watengwe." 2:9 *Pia anaitwa Kalebui katika mstari wa 18, 19, na 42. 2:18 *Pia anaitwa Kelubai katika mstari wa 9.

SURA YA 2

a Yos 7:15, 18

b Kum 7:26
Yos 6:18
Yos 22:20

c 1Sa 27:10

d Ru 4:19-21
Mt 1:3

e Mt 1:4, 5

f Hes 2:3

g Lu 3:23, 32

h Ru 2:1

i Ru 4:17, 22
1Sa 16:1

j 1Sa 17:13

k 1Sa 16:6-10

l 1Sa 16:13
1Sa 17:12
Mt 1:6

m 2Sa 17:25

n 2Sa 21:17
2Sa 23:18, 19o 2Sa 8:16
1Nya 11:6p 2Sa 2:18
2Sa 3:30
2Sa 23:24q 2Sa 19:13
1Fa 2:5

r 1Nya 4:4

Safu ya 2

a Kut 17:12
Kut 24:14b Kut 31:2-5
Kut 36:1
Kut 37:1c Mwa 50:23
1Nya 7:14d Hes 26:29
Yos 17:1e Kum 3:14
Yos 13:29, 30

f Hes 32:40, 41

g 2Sa 3:3
2Sa 13:38

h 2Sa 8:6

i 1Fa 4:13

j Hes 32:42

k Mwa 46:12

l 1Nya 4:5

m Ne 3:5

lia Kalebu mwana aliyelitwa Huru.^a 20 Huru akamzaa Uri. Uri akamzaa Bezaleli.^b

21 Baadaye Hezroni akalala na binti ya Makiri^c baba ya Gileadi.^d Hezroni alikuwa na umri wa miaka 60 alipomwoa, naye akamzalia Segubu. 22 Segubu akamzaa Yairi,^e aliyekuwa na majiji 23 katika nchi ya Gileadi.^f 23 Baadaye Geshuri^g na Siria^h wakachukua Hawoth-yairiⁱ kutoka kwao, pamoja na Kenathi^j na miji yake, majiji 60. Wote hao walikuwa wazao wa Makiri baba ya Gileadi.

24 Baada ya Hezroni^k kufa huko Kalebu-efratha, Abiya mke wake alimzalia Hezroni mwana aliyelitwa Ashuri,^l baba ya Tekoa.^m

25 Wana wa Yerahmeeli mzaliwa wa kwanza wa Hezroni walikuwa Ramu mzaliwa wa kwanza, Buna, Oreni, Ozemu, na Ahiya. 26 Yerahmeeli alikuwa na mke mwingine aliyelitwa Atara. Alikuwa mama ya Onamu. 27 Wana wa Ramu mzaliwa wa kwanza wa Yerahmeeli walikuwa Maazi, Yamini, na Ekeri. 28 Wana wa Onamu walikuwa Shamai na Yada. Wana wa Shamai walikuwa Nadabu na Abishuri. 29 Mke wa Abishuri aliitwa Abihaili, alimzalia Abishuri wana walioitwa Abani na Molidi. 30 Wana wa Nadabu walikuwa Seledi na Apaimu. Lakini Seledi alikufa bila watoto.[#] 31 Mwana* wa Apaimu alikuwa Ishi. Na mwana[#] wa Ishi alikuwa Sheshani, na mwana[#] wa Sheshani aliku-

2:30, 31 *Tnn., "wana."

wa Alai. **32** Wana wa Yada ndugu ya Shamai walikuwa Yetheri na Yonathani. Lakinini Yetheri alikufa bila watoto.* **33** Wana wa Yonathani walikuwa Pelethi na Zaza. Hao ndio waliokuwa wazao wa Yerahmeeli.

34 Sheshani hakuwa na watoto wa kiume, alikuwa na mabinti tu. Sheshani alikuwa na mtumishi Mmisri aliyetiwa Yarha. **35** Sheshani akamchukua binti yake na kumpa Yarha mtumishi wake awe mke wake, na binti huyo akamzalia mwana aliyetiwa Atai. **36** Atai akamzaa Nathani. Nathani akamzaa Zabadi. **37** Zabadi akamzaa Eflali. Eflali akamzaa Obedi. **38** Obedi akamzaa Yehu. Yehu akamzaa Azaria. **39** Azaria akamzaa Helezi. Helezi akamzaa Eleasa. **40** Eleasa akamzaa Sismai. Sismai akamzaa Shalumu. **41** Shalumu akamzaa Yekamia. Yekamia akamzaa Elishama.

42 Wana wa Kalebu*^a ndugu ya Yerahmeeli walikuwa Meshu mzaliwa wake wa kwanza, aliyekuwa baba ya Zifu, na wana wa Maresha baba ya Hebroni. **43** Wana wa Hebroni walikuwa Kora, Tapua, Rekemu, na Shema. **44** Shema akamzaa Rahamu baba ya Yorkeamu. Rekemu akamzaa Shamai. **45** Mwana wa Shamai alikuwa Maoni. Maoni alikuwa baba ya Beth-suri.^b **46** Efa suria wa Kalebu alimzaa Harani, Mosa, na Gazezi. Harani akamzaa Gazezi. **47** Wana wa Yahdai walikuwa Regemu, Yothamu, Geshani, Peleti, Efa, na Shaafu.

2:32 *Tnn., "wana." 2:42 *Pia anaitwa Kelubai katika mstari wa 9.

SURA YA 2

a 1Nya 2:9

b Yos 15:20, 58
Ne 3:16

Safu ya 2

a Yos 15:21, 31

b Yos 15:20, 57

c 1Nya 2:18

d Yos 15:16, 17

e Kut 17:12
Kut 24:14

f 1Nya 2:19

g Yos 15:9, 12
1Nya 13:5h Mwa 35:19
Yoh 7:42

i 1Nya 11:10, 40

j 1Nya 4:2

k Yos 15:20, 33

l Mwa 35:19
Mt 2:1m Amu 1:16
Amu 4:11
1Sa 15:6n 2Fa 10:15
Yer 35:6, 19

SURA YA 3

o 2Sa 3:2-5

p 2Sa 13:32

q 1Sa 25:43

r 1Sa 25:2, 39

s 2Sa 13:28, 37
2Sa 15:10
2Sa 18:14t 1Fa 1:5, 11
1Fa 2:24

1 MAMBO YA NYAKATI 2:32-3:4

48 Maaka suria wa Kalebu alimzaa Sheberi na Tirhana. **49** Baada ya muda akamzaa Shaafu baba ya Madmana^a na Sheva baba ya Makbena na Gibea.^b Binti ya Kalebu^c alikuwa Aksa.^d **50** Hao ndio waliokuwa wazao wa Kalebu.

Wana wa Huru^e mzaliwa wa kwanza wa Efratha^f walikuwa Shobali baba ya Kiriath-yearimu,^g **51** Salma baba ya Bethlehemu,^h na Harefu baba ya Bethgaderi. **52** Shobali baba ya Kiriath-yearimu alikuwa na wana hawa: Haroe na nusu ya watu wa Menuhothi. **53** Koo za Kiriath-yearimu zilikuwa Waithri,ⁱ Waputhu, Washumathi, na Wamishra. Wasorathi^j na Waeshtaoli^k walitokana na koo hizo. **54** Wana wa Salma walikuwa Bethlehemu,^l Wanetofa, Atroth-beth-yoabu, na nusu ya Wamanahathi, na Wazori. **55** Koo za waandishi walioishi Yabesi zilikuwa Watirathi, Washimea, na Wasukathi. Hao walikuwa Wakeni^m wazao wa Hamathi baba wa nyumba ya Rekabu.ⁿ

3 Hawa ndio wana wa Daudi waliozaliwa Hebroni:^o mzaliwa wa kwanza aliitwa Amnoni,^p mama yake aliitwa Ahinoamu^q kutoka Yezreeli; wa pili, Danieli, mama yake aliitwa Abigaili^r Mkarmeli; **2** wa tatu, Absalomu,^s mwana wa Maaka binti ya Talmi mfalme wa Geshuri; wa nne, Adoniya^t mwana wa Hagithi; **3** wa tano, Shefatia, ambaye mama yake aliitwa Abitali; na wa sita, Ithreamu, ambaye mama yake aliitwa Eglu, mke wa Daudi. **4** Aliwazaa

wana hao sita kule Hebroni; alitawala huko kwa miaka 7 na miezi 6, naye alitawala kule Yerusalemu kwa miaka 33.^a

5 Aliwazaa wana wafuatao huko Yerusalemu:^b Shimea, Shobabu, Nathani,^c na Sulemani;^d mama ya wana hao wanne alikuwa Bath-sheba^e binti ya Amieli. **6** Alikuwa na wana wengine tisa ambao ni Ibhari, Elishama, Elifeleti, **7** Noga, Nefegi, Yafia, **8** Elishama, Eliada, na Elifeleti. **9** Hao wote walikuwa wana wa Daudi, bila kuhesabu wana wa masuria, na dada yao alikuwa Tamari.^f

10 Mwana wa Sulemani alikuwa Rehoboamu;^g mwana wa Rehoboamu alikuwa Abiya,^h mwana wa Abiya alikuwa Asa,ⁱ mwana wa Asa alikuwa Yehoshafati,^j **11** mwana wa Yehoshafati alikuwa Yehoram,^k mwana wa Yehoram alikuwa Ahazia,^l mwana wa Ahazia alikuwa Yehoashi,^m **12** mwana wa Yehoashi alikuwa Amasia,ⁿ mwana wa Amasia alikuwa Azaria,^o mwana wa Azaria alikuwa Yothamu,^p **13** mwana wa Yothamu alikuwa Ahazi,^q mwana wa Ahazi alikuwa Hezekia,^r mwana wa Hezekia alikuwa Manase,^s **14** mwana wa Manase alikuwa Amoni,^t mwana wa Amoni alikuwa Yosia.^u **15** Wana wa Yosia walikuwa Yohanani mzaliwa wa kwanza, wa pili, Yehoyakimu,^v wa tatu, Sedekia,^w wa nne, Shalumu. **16** Wana wa Yehoyakimu walikuwa Yekonia^x mwanawe na Sedekia mwana wa Yekonia. **17** Wana wa Yekonia aliyekuwa mfungwa walikuwa Shealtiel, **18** Malkiram, Pedaya, Shenazari, Yekamia, Hoshama, na Nedabia. **19** Wana wa

SURA YA 3

- a 2Sa 5:5
b 2Sa 5:13-16
1Nya 14:3-7
c Lu 3:23, 31
d Mt 1:7
e 2Sa 11:3, 27
f 2Sa 13:1
g 1Fa 11:43
h 2Nya 13:1
i 2Nya 14:1
j 2Nya 20:31
k 2Nya 21:5
l 2Nya 22:2
m 2Nya 24:1
n 2Nya 25:1
o 2Fa 14:21
p 2Nya 27:1
q 2Nya 28:1
r 2Nya 29:1
s 2Fa 21:1
t 2Fa 21:19
u 2Fa 22:1
v 2Fa 23:34
2Nya 36:5
w 2Fa 24:17
2Nya 36:11
x 2Fa 24:6, 8
2Fa 25:27
Est 2:6

Safu ya 2

- a Ezi 5:2
Mt 1:12
Lu 3:23, 27

SURA YA 4

- b Mwa 38:29
Hes 26:20
Ru 4:18
Mt 1:3
c Mwa 46:12
1Nya 2:5
d Kut 17:12
Kut 24:14
1Nya 2:19
e 1Nya 2:50
f 1Nya 2:53
g 2Nya 11:5, 6
h 1Nya 2:19
i Mik 5:2
j 1Nya 2:24
k 2Nya 11:5, 6

Pedaya walikuwa Zerubabeli^a na Shimei; na wana wa Zerubabeli walikuwa Meshulamu na Hanania (na dada yao alikuwa Shelomithi); **20** naye alikuwa na wana wengine watano ambao ni Hashuba, Oheli, Berekia, Hasadia, na Yushab-hesedi. **21** Wana wa Hanania walikuwa Pelatia na Yeshaya; mwana* wa Yeshaya alikuwa Refaya; mwana* wa Refaya alikuwa Arnani; mwana* wa Arnani alikuwa Obadia; mwana* wa Obadia alikuwa Shekania; **22** na wana wa Shekania walikuwa Shemaya na wana wa Shemaya walikuwa Hatushi, Igali, Baria, Nearia, na Shafati—jumla ya wana sita. **23** Na wana wa Nearia walikuwa Elioenai, Hizkia, na Azrikamu, wana watatu. **24** Na wana wa Elioenai walikuwa Hodavia, Eliashibu, Pelaya, Akubu, Yohanani, Delaya, na Anani, wana saba.

4 Wana wa Yuda walikuwa Perezi,^b Hezroni,^c Karmi, Huru,^d na Shobali.^e **2** Reaya mwana wa Shobali alimzaa Yahathi; Yahathi akamzaa Ahumai na Lahadi. Hizo ndizo zilizokuwa koo za Wasorathi.^f **3** Hawa ndio waliokuwa wana wa baba ya Etamu:^g Yezreeli, Ishma, na Idbashi (na dada yao aliitwa Haseleponi), **4** Penueli alimzaa Gedori, na Ezeri akamzaa Husha. Hao ndio waliokuwa wana wa Huru,^h mzaliwa wa kwanza wa Efratha na baba ya Bethlehemu.ⁱ **5** Ashuri^j baba ya Tekoa^k alikuwa na wake wawili, Hela na Naara. **6** Naara akamzalia Ashuri wana hawa: Ahuzamu, Heferi, Temeni, na

3:21 * Tnn., "wana."

Haahashtari. Hao ndio waliokuwa wana wa Naara. **7** Na wana wa Hela walikuwa Serethi, Ishari, na Ethnani. **8** Kosi alimzaa Anubu, Zobebe, na familia za Aharheli mwana wa Harumi.

9 Yabesi aliheshimiwa sana kuliko ndugu zake; na mama yake alimwita jina Yabesi, aki-sema: "Nilimzaa kwa uchungu."* **10** Yabesi akamililia Mungu wa Israeli, akisema: "Laiti ungenibariki na kupanua eneo langu na kuuruhusu mkono wako uwe pamoja nami na kuniokoa kutoka katika msiba, ili msiba huo usinidhuruli!" Basi Mungu akatimiza ombi lake.

11 Kelubu ndugu ya Shuha akamzaa Mehiri, aliyekuwa baba ya Eshtoni. **12** Eshtoni akamzaa Beth-rafa, Pasea, na Tehina, baba ya Ir-nahashi. Hao ndio waliokuwa wanaume wa Reka. **13** Na wana wa Kenasi walikuwa Othnieli^a na Seraya, na mwana* wa Othnieli alikuwa Hathathi. **14** Meo-nothai akamzaa Ofra. Seraya akamzaa Yoabu baba ya Ge-harashimu,* walipewa jina hilo kwa sababu walikuwa mafundi.

15 Wana wa Kalebub mwana wa Yefune walikuwa Iru, Ela, na Naamu; na mwana* wa Ela alikuwa Kenasi. **16** Wana wa Yehaleleli walikuwa Zifu, Zifa, Tiria, na Asareli. **17** Wana wa Ezra walikuwa Yetheri, Meredi, Eferi, na Yaloni; alishika* mimba na kumzaa Miria-

4:9 *Huenda jina Yabesi linahusiana na neno la Kiebrania linalomaanisha "uchungu." 4:13, 15 *Tnn., "wana." 4:14 *Maana yake "Bonde la Mafundi." 4:17 *Inawezekana ni Bithia anayetajwa katika mstari wa 18.

SURA YA 4

a Yos 15:16,17
Amu 3:9,11

b Hes 32:11,12
Yos 15:13

Safu ya 2

a Mwa 38:2,5
Hes 26:20

b Mwa 46:10

c Hes 26:12,13

d Hes 26:22

mu, Shamai, na Ishba baba ya Eshtemoa. **18** (Na mke wake Myahudi alimzaa Yeredi baba ya Gedori, Heberi baba ya Soko, na Yekuthieli baba ya Zanoa.) Hao ndio waliokuwa wana wa Bithia, binti ya Farao, aliyeolewa na Meredi.

19 Wana wa mke wa Hodia, dada ya Nahamu, walikuwa baba za Keila Mgarini na Eshtemoa Mmaakathi. **20** Na wana wa Shimoni walikuwa Amnoni, Rina, Benhanani, na Tiloni. Na wana wa Ishi walikuwa Zohethi na Benzohethi.

21 Wana wa Shela^a mwana wa Yuda walikuwa Eri baba ya Leka, Laada baba ya Maresha, na familia za wafumaji wa vitambaa bora wa nyumba ya Ashbea, **22** na Yokimu, wanaume wa Kozeba, Yoashi, na Sarafi, waliowaoa wana-wake Wamoabu, na Yashubilehemu. Habari hizi ni za zamani za kale.* **23** Hao ndio wafinyanzi walioishi Netaimu na Gedera. Waliishi huko na kumtumikia mfalme.

24 Wana wa Simeoni^b walikuwa Nemueli, Yamini, Yarithu, Zera, na Shauli.^c **25** Mwana wa Shauli alikuwa Shalumu, mwana wa Shalumu alikuwa Mibsamu, na mwana wa Mibsamu alikuwa Mishma. **26** Na wana wa Mishma walikuwa Hamueli, Zakuri mwana wa Hamueli, na Shimei mwana wa Zakuri. **27** Na Shimei alikuwa na wana 16 na mabinti 6; lakini ndugu zake hawakuwa na wana wengi, na hakuna familia yao yoyote iliyokuwa na wana wengi kama wanaume wa Yuda.^d

4:22 *Au "Maneno haya ni ya utamaduni wa kale."

28 Waliishi Beer-sheba,^a Molada,^b Hasar-shuali,^c **29** Bilha, Esemu,^d Toladi, **30** Bethueli,^e Horma,^f Siklagi,^g **31** Beth-markabothi, Hasar-susimu,^h Beth-biri, na Shaaraimu. Hayo yalikuwa majiji yao mpaka wakati wa utawala wa Daudi.

32 Waliishi Etamu, Aini, Rimoni, Tokeni, na Ashani,ⁱ majiji matano, **33** pamoja na vijiji vyao vilivyozunguka majiji hayo mpaka Baali. Hizo ndizo orodha za koo zao zilizoandikishwa na mahali walipoishi. **34** Na Meshobabu, Yamleki, Yosha mwana wa Amazia, **35** Yoeli, Yehu mwana wa Yoshihia mwana wa Seraya mwana wa Asieli, **36** na Elioenai, Yaakoba, Yeshohaya, Asaya, Adieli, Yesimieli, Benaya, **37** na Ziza mwana wa Shifi mwana wa Aloni mwana wa Yedaya mwana wa Shimri mwana wa Shemaya; **38** watu hao waliotajwa kwa majina walikuwa wakuu katika koo zao, na idadi ya watu katika nyumba ya mababu zao iliongezeka. **39** Nao walionda kwenye njia ya kuingia Gedori, upande wa mashariki wa bonde, ili kutafuta malisho ya wanyama wao. **40** Hatimaye walipata malisho mazuri yenye majani mengi, na nchi ilikuwa kubwa, yenye utulivu, na amani. Wahamu ndio waliishi katika nchi hiyo awali. **41** Watu hao ambao majina yao yameorodheshwa walikuja katika siku za utawala wa Mfalme Hezekia^k wa Yuda, wakayabomoa mahema ya Wahamu na Wameunimu waliokuwa huko. Waliwaangamiza tangu siku hiyo; wakachukua eneo lao kwa sababu lilikuwa

SURA YA 4

a Yos 19:1, 2

b Yos 15:21, 26

c Yos 15:21, 28
Yos 19:1, 3
Ne 11:25-27

d Yos 15:21, 29

e Yos 19:1, 4

f Amu 1:17

g Yos 15:20, 31
Yos 19:1, 5
1Sa 27:5, 6

h Yos 19:1, 5

i Yos 19:1, 7

j Mwa 10:6, 20

k 2Nya 29:1

Safu ya 2

a Mwa 36:8

b Kut 17:14, 16
1Sa 15:7

SURA YA 5

c Mwa 29:32
Mwa 49:3, 4

d Mwa 35:22

e Mwa 49:22, 26
Yos 14:4f Mwa 49:8, 10
Hes 2:3
Hes 10:14
Amu 1:1, 2
Zb 60:7g Mt 2:6
Ebr 7:14h Mwa 46:9
Kut 6:14

i 2Fa 16:7

na malisho kwa ajili ya wanyama wao.

42 Baadhi ya watu wa kabila la Simeoni, wanaume 500, walienda kwenye Mlima Seiri^a wakiwa na Pelatia, Nearia, Refaya, na Uzieli, wana wa Ishi ambao waliwaongoza. **43** Kisha wakawaangamiza Waamaleki^b waliobaki ambao walikuwa wametoroka, nao wamekuwa wakiishi huko mpaka leo.

5 Hawa ndio wana wa Rubeni,^c mzaliwa wa kwanza wa Israeli. Yeye ndiye aliyekuwa mzaliwa wa kwanza, lakini kwa sababu alikichafua* kitanda cha baba yake,^d haki yake ya mzaliwa wa kwanza walipewa wana wa Yosefu^e mwana wa Israeli, kwa hiyo hakuandikishwa katika orodha ya ukoo kwamba ana haki ya mzaliwa wa kwanza. **2** Ingawa Yuda^f alikuwa mkuu kuliko ndugu zake na kiongozi alitoka kwake,^g haki ya mzaliwa wa kwanza ilikuwa ya Yosefu. **3** Wana wa Rubeni mzaliwa wa kwanza wa Israeli walikuwa Hanoki, Palu, Hezroni, na Karmi.^h **4** Wana wa Yoeli walikuwa Shemaya mwana-we, Gogu mwana wa Shemaya, Shimei mwana wa Gogu, **5** Mika mwana wa Shimei, Reaya mwana wa Mika, Baali mwana wa Reaya, **6** na Beera mwana wa Baali, ambaye Mfalme Tilgath-pilneseriⁱ wa Ashuru alimpeleka uhamishoni; alikuwa mkuu wa Warubeni. **7** Ndugu zake walioandikishwa katika orodha ya koo kulingana na koo zao na kulingana na wazao wao walikuwa, Yeieli, aliyekuwa kiongozi wao, Zekaria, **8** na Bela

5:1 *Au "alikitia unajisi."

mwana wa Azazi mwana wa Shema mwana wa Yoeli, aliyeishi Aroeri^a mpaka Nebo na Baal-meoni.^b **9** Naye aliishi upande wa mashariki mpaka mahali ambapo nyika inaanzia kwenye Mto Efrati,^c kwa maana mifugo yao ilikuwa imeongezeka sana katika nchi ya Gileadi.^d **10** Katika siku za utawala wa Sauli, walipigana vita na Wahagri, nao wakawashinda, wakakaa katika mahe-ma yao kwenye eneo lote lililo upande wa mashariki wa Gileadi.

11 Wazao wa Gadi waliishi karibu nao katika nchi ya Bashani mpaka kule Saleka.^e **12** Yoeli ndiye aliyekuwa kiongozi wao, Shafamu alikuwa wa pili, na Yanai na Shafati walikuwa viongozi kule Bashani. **13** Na ndugu zao wa koo* zao walikuwa Mikaeli, Meshulamu, Sheba, Yorai, Yakani, Zia, na Eberi, jumla ya watu saba. **14** Hao ndio waliokuwa wana wa Abihaili mwana wa Huri mwana wa Yaroa mwana wa Gileadi mwana wa Mikaeli mwana wa Yeshishai mwana wa Yahdo mwana wa Abdieli mwana wa Guni alikuwa kiongozi wa ukoo wao.* **16** Waliishi Gileadi,^f kule Bashani^g na katika miji yake, na katika malisho yote ya Sharoni kufikia mipakani mwake. **17** Wote waliandikishwa kulingana na koo zao katika siku za utawala wa Mfalme Yothamu^h wa Yuda na katika siku za utawala wa Mfalme Yeroboamu*ⁱ wa Israeli.

18 Watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la

5:13, 15, 24 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 5:17 *Yaani, Yeroboamu wa Pili.

SURA YA 5

a Kum 2:36

b Hes 32:34, 38
Yos 13:15, 17
Eze 25:9, 10c Mwa 15:18
Kum 1:7
Yos 1:4
2Sa 8:3

d Yos 22:9

e Kum 3:8, 10
Yos 12:4, 5

f Hes 32:1

g Kum 3:3, 13
Kum 32:14h 2Fa 15:32
2Nya 27:1
Isa 1:1
Ho 1:1
Mik 1:1

i 2Fa 14:16, 28

Safu ya 2

a 1Nya 5:10

b Mwa 25:13, 15
1Nya 1:31c Zb 20:7
Zb 22:4d Yos 10:42
1Sa 17:45, 47
2Nya 20:15e 2Fa 15:29
2Fa 17:6

f Yos 13:29, 30

g Kum 4:47, 48

h Kum 5:7-9
Amu 2:17
Amu 8:33
2Fa 17:10, 11i Ezi 1:1
Met 21:1

Manase walikuwa na mashujaa hodari 44,760 katika jeshi lao waliobeba ngao na mapanga na kujihami kwa pinde,* nao walikuwa wamezoezwa kwa ajili ya vita. **19** Walipigana vita na Wahagri,^a Wayeturi, Wanafishi,^b na Wanodabu. **20** Mungu aliwasaidia kupigana nao, akawatia mikononi mwao Wahagri na wote waliokuwa pamoja nao, kwa maana walimwomba Mungu awasaidie vitani, akasiliza maombi yao kwa sababu walimumaini.^c **21** Waliteka nyara mifugo yao—ngamia 50,000, kondoo 250,000, na punda 2,000—na pia watu 100,000. **22** Wengi waliuawa, kwa sababu Mungu wa kweli ndiye aliyepigana vita hivyo.^d Nao waliendelea kuishi katika nchi yao mpaka walipopoleleka uhamishoni.^e

23 Wazao wa nusu ya kabila la Manase^f waliishi katika nchi hiyo kuanzia Bashani mpaka Baal-hermoni na Seniri na Mlima Hermoni.^g Walikuwa wengi sana. **24** Hawa ndio waliokuwa viongozi wa koo* zao: Eferi, Ishi, Elieli, Azrieli, Yeremia, Hodavia, na Yahdieli; walikuwa mashujaa hodari, wanaume maarufu, na viongozi wa koo* zao. **25** Lakini hawakutenda kwa uaminifu kumwelekea Mungu wa mababu zao, wakafanya ukahaba na miungu ya mataifa yaliyokuwa nchini,^h mataifa ambayo Mungu alikuwa ameyaaangamiza kutoka mbele yao. **26** Kwa hiyo Mungu wa Israeli akaichochea roho ya Mfalme Pulu wa Ashuruⁱ (yaani, Mfalme

5:18 *Tnn., "na kukunyaga upinde."

Tilgath-pilneseri^a wa Ashuru hivi kwamba akawapeleka uhamishoni watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase, akawapeleka Hala, Habori, Hara, na mto Gozani,^b nao wako huko hadi leo.

6 Wana wa Lawi^c walikuwa Gershoni, Kohathi,^d na Merari.^e **2** Wana wa Kohathi walikuwa Amramu, Ishari,^f Hebroni, na Uzieli.^g **3** Watoto* wa Amramu^h walikuwa Haruni,ⁱ Musa,^j na pia Miriamu.^k Na wana wa Haruni walikuwa Nadabu, Abihu,^l Eleazari,^m na Ithamari.ⁿ **4** Eleazari alimzaa Finehasi;^o Finehasi akamzaa Abishua. **5** Abishua akamzaa Buki; Buki akamzaa Uzi. **6** Uzi akamzaa Zeraya; Zeraya akamzaa Merayothi. **7** Merayothi akamzaa Amaria; Amaria akamzaa Ahitubu.^p **8** Ahitubu akamzaa Sadoki;^q Sadoki akamzaa Ahimaazi.^r **9** Ahimaazi akamzaa Azaria; Azaria akamzaa Yohanani. **10** Yohanani akamzaa Azaria. Alitumikia akiwa kuhani katika nyumba ambayo Sulemani alijenga Yerusalemu.

11 Azaria akamzaa Amaria; Amaria akamzaa Ahitubu. **12** Ahitubu akamzaa Sadoki;^s Sadoki akamzaa Shalumu. **13** Shalumu akamzaa Hilkiya;^t Hilkiya akamzaa Azaria. **14** Azaria akamzaa Seraya;^u Seraya akamzaa Yehosadaki.^v **15** Na Yehosadaki alipeleka uhamishoni wakati Yehova alipowapeleka watu wa Yuda na Yerusalemu uhamishoni kwa mkono wa Nebukadnezar.

6:3 *Tnn., "Wana."

SURA YA 5

a 2Fa 15:19, 29
b 2Fa 17:6
2Fa 18:11

SURA YA 6

c Mwa 29:34
Kut 6:16
d Kut 6:18
Hes 3:27
e Hes 3:17
Hes 26:57
f Kut 6:21
g Kut 6:22
Law 10:4
h Kut 6:20
i 1Nya 23:13
j Kut 6:26
Mdo 7:37, 38
k Kut 15:20
l Kut 24:1
Law 10:1
m Hes 3:32
Kum 10:6
n Kut 6:23
Kut 28:1
Hes 4:28
1Nya 24:2, 4
o Kut 6:25
Hes 25:11
p 2Sa 8:17
q 1Fa 1:8
1Fa 2:35
r 2Sa 15:27, 36
s Ne 11:11
t 2Nya 34:14
u 2Fa 25:18
v Hag 1:1

Safu ya 2

a Hes 3:18
b Hes 3:19, 20
c Hes 26:57
d Hes 3:18
e Hes 16:1, 32
Hes 26:10, 11
Yud 11
f Kut 6:24
g 1Sa 1:1
h 1Sa 1:20
i 1Sa 8:1, 2
j Kut 6:19
1Nya 23:21

16 Wana wa Lawi walikuwa Gershomu,* Kohathi, na Merari. **17** Haya ndiyo majina ya wana wa Gershomu: Libni na Shimei.^a **18** Wana wa Kohathi walikuwa Amramu, Ishari, Hebroni, na Uzieli.^b **19** Wana wa Merari walikuwa Mali na Mushi.

Hizi ndizo zilizokuwa koo za Walawi kulingana na mababu zao:^c **20** kutoka katika ukoo wa Gershomu,^d Libni mwana wa Gershomu, Yahathi mwana wa Libni, Zima mwana wa Yahathi, **21** Yoa mwana wa Zima, Ido mwana wa Yoa, Zera mwana wa Ido, Yeatherai mwana wa Zera. **22** Wana* wa Kohathi walikuwa Aminadabu mwanawe, Kora^e mwana wa Aminadabu, Eliri mwana wa Kora, **23** Elkana mwana wa Asiri, Ebiasafu^f mwana wa Elkana, Asiri mwana wa Ebiasafu, **24** Tahathi mwana wa Asiri, Urieli mwana wa Tahathi, Uzia mwana wa Urieli, na Shauli mwana wa Uzia. **25** Wana wa Elkana walikuwa Amasai na Ahimothi. **26** Kwa habari ya Elkana, wana wa Elkana walikuwa Zofai mwanawe, Nahathi mwana wa Zofai, **27** Eliabu mwana wa Nahathi, Yerohamu mwana wa Eliabu, Elkana^g mwana wa Yerohamu. **28** Wana wa Samweli^h walikuwa Yoeli mzaliwa wa kwanza na wa pili Abiya.ⁱ **29** Wana* wa Merari walikuwa Mali,^j Libni mwana wa Mali, Shimei mwana wa Libni, Uza mwana wa Shimei, **30** Shimei mwana wa Uza, Haggia mwana wa Shimei, na Asaya mwana wa Haggia.

6:16 *Pia anaitwa Gershoni katika mstari wa 1. 6:22, 29 *Au "Wazao."

31 Hao ndio watu ambao Daudi aliwaweka ili waongoze uimbaji katika nyumba ya Yehova baada ya Sanduku kuletwa likae* humo.^a **32** Ndio waliokuwa na jukumu la kusimamia uimbaji katika hema la ibada, yaani, hema la mkutano mpaka Sulemani alipojenga nyumba ya Yehova huko Yerusalemu,^b nao walitekeleza utumishi wao kulingana na maagizo waliyopewa.^c **33** Hawa ndio wanau-me waliotumikia pamoja na wana wao: kutoka katika ukoo wa Wakohathi, Hemani^d mwiimbaji, mwana wa Yoeli^e mwana wa Samweli **34** mwana wa Elkana^f mwana wa Yerohamu mwana wa Elieli mwana wa Toa **35** mwana wa Sufu mwana wa Elkana mwana wa Mahathi mwana wa Amasai **36** mwana wa Elkana mwana wa Yoeli mwana wa Azaria mwana wa Sefania **37** mwana wa Tahathi mwana wa Asiri mwana wa Ebiasafu mwana wa Kora **38** mwana wa Ishari mwana wa Kohathi mwana wa Lawi mwana wa Israeli.

39 Asafu^g ndugu yake alisimama kwenye mkono wake wa kulia; Asafu alikuwa mwana wa Berekia mwana wa Shimea **40** mwana wa Mikaeli mwana wa Baaseya mwana wa Malkiya **41** mwana wa Ethni mwana wa Zera mwana wa Adaya **42** mwana wa Ethani mwana wa Zima mwana wa Shimei **43** mwana wa Yahathi mwana wa Gershomu mwana wa Lawi.

44 Wazao wa Merari^h ndugu zao walikuwa kwenye mkono wake wa kushoto; kulikuwa na

SURA YA 6

a 2Sa 6:17
1Nya 15:16

b 1Fa 6:14

c 2Nya 35:15

d 1Nya 15:16, 17

e 1Sa 8:1, 2

f 1Sa 1:1

g 1Nya 25:1
2Nya 5:12
Zb 50:Uta

h 1Nya 23:6

Safu ya 2

a 1Nya 15:16, 17

b Hes 3:5-7

c Kut 28:1
Hes 3:10

d Kut 29:38

e Kut 30:7

f Kut 30:10
Law 4:20
Law 17:11
2Nya 29:24

g Kut 6:23

h Kut 28:1
Hes 3:32

i 2Sa 8:17

j 1Fa 2:35

k Hes 13:22
Yos 21:8, 11

Ethani^a mwana wa Kishi mwana wa Abdi mwana wa Maluku **45** mwana wa Hashabia mwana wa Amazia mwana wa Hilikia **46** mwana wa Amzi mwana wa Bani mwana wa Shemeri **47** mwana wa Mali mwana wa Mushi mwana wa Merari mwana wa Lawi.

48 Ndugu zao Walawi waliwekwa* ili watekeleze utumishi wote wa hema la ibada, nyumba ya Mungu wa kweli.^b **49** Haruni na wanawe^c walifukiza moshi wa dhabihu kwenye madhabahu ya dhabihu ya kuteketezwa^d na kwenye madhabahu ya uvumba,^e wakitekeleza majukumu yaliyohusiana na vitu vitakatifu kabisa, ili kufunika dhambi za Waisraeli,^f kulingana na yote ambayo Musa mtumishi wa Mungu wa kweli alikuwa ameamuru. **50** Hawa ndio waliokuwa wazao wa Haruni:^g Eleazari mwanawe, Finehasi mwana wa Eleazari,^h Abishua mwana wa Finehasi, **51** Buki mwana wa Abishua, Uzi mwana wa Buki, Zeraya mwana wa Uzi, **52** Merayothi mwana wa Zeraya, Amaria mwana wa Merayothi, Ahitubuⁱ mwana wa Amaria, **53** Sadoki^j mwana wa Ahitubu, na Ahimaazi mwana wa Sadoki.

54 Haya ndiyo yaliyokuwa makao yao kulingana na kamibi zao* katika eneo lao: wazao wa Haruni waliokuwa wa ukoo wa Wakohathi, waliangukiwa na kura ya kwanza, **55** waliwapa Hebroni^k katika nchi ya Yuda, pamoja na malisho yake. **56** Lakini

6:48 *Tnn., "walitolewa." **6:54** *Au "kambi zao zilizozingirwa na kuta."

mashamba ya jiji na vijiji vya-
ke walimpa Kalebu^a mwa-
na wa Yefune. **57** Na wazao
wa Haruni walipewa majiji
haya ya* makimbilio:^b Hebro-
ni,^c na pia Libna^d na malisho
yake, Yatiri,^e Eshtemoa na ma-
lisho yake,^f **58** Hileni na ma-
lisho yake, Debiri^g na malisho
yake, **59** Ashani^h na malisho
yake, na Beth-shemeshiⁱ na
malisho yake; **60** na kutoka
katika kabila la Benjamini,
Geba^j na malisho yake, Aleme-
thi na malisho yake, na Ana-
thothi^k na malisho yake. Maji-
ji yao yote kwa ajili ya koo zao
yalikuwa majiji 13.^l

61 Wakohathi waliobaki wa-
lipewa* majiji kumi, kutoka
katika ukoo wa kabila, kuto-
ka katika nusu ya kabila, nusu
ya kabila la Manase.^m

62 Wagershomu kulingana
na koo zao walipewa majiji 13
kutoka katika kabila la Isakari,
kabila la Asheri, kabila la
Naftali, na kabila la Manase
kule Bashani.ⁿ

63 Wamerari kulingana na
koo zao walipewa majiji 12 ku-
toka katika kabila la Rubeni,
kabila la Gadi, na kabila la Za-
buloni.^o

64 Kwa hiyo Waisraeli wali-
wapa Walawi majiji hayo
na malisho yake.^p **65** Isito-
she, waliwapa kwa kura ma-
jiji hayo kutoka katika kabila
la Yuda, kabila la Simeoni, na
kabila la Benjamini, ambayo
yametajwa majina yao.

66 Baadhi ya koo za Wako-
hathi zilipewa majiji kutoka
katika kabila la Efraimu, yaka-
wa maeneo yao.^q **67** Waliwa-

6:57 *Au labda, "jiji hili la," kulingana
na Yos 21:13. 6:61 *Au "walipewa kwa
kura."

SURA YA 6

a Yos 14:13

Amu 1:20

b Hes 35:12,13

c Yos 20:7,9

d Yos 15:20,42

e Yos 15:20,48

f Yos 21:13-16

g Amu 1:11

h 1Nya 4:24,32

i Yos 15:10,12

j Yos 18:21,24

k Yos 21:8,18

Yer 1:1

l Yos 21:4

m Yos 21:5

n Yos 21:27-33

o Yos 21:34-40

p Hes 35:2-4

q Yos 21:20-26

Safu ya 2

a Yos 20:7,9

b Yos 16:10

c Yos 10:11

d Yos 10:12

Amu 1:35

e Yos 19:45,48

f Kum 4:41-43

g Yos 21:27

h Yos 19:12,16

i Yos 21:8,28

j Yos 21:8,30

k Yos 19:28,31

Amu 1:31

l Yos 20:7,9

Yos 21:32,33

m Mt 3:13

n Yos 21:34-39

o Hes 21:23

p Kum 2:26

pa majiji ya* makimbilio, She-
kemu^a na malisho yake kati-
ka eneo lenye milima la Efrai-
mu, Gezeri^b na malisho yake,
68 Yokmeamu na malisho
yake, Beth-horoni^c na malisho
yake, **69** Aiyaloni^d na mali-
sho yake, na Gath-rimoni^e na
malisho yake; **70** na koo zi-
lizobaki za Wakohathi zilipe-
wa kutoka katika nusu ya ka-
bila la Manase, Aneri na mali-
sho yake na Bileamu na mali-
sho yake.

71 Wagershomu walipewa
kutoka katika ukoo wa nusu
ya kabila la Manase, Golani^f
kule Bashani na malisho yake
na Ashtarothi na malisho
yake;^g **72** na kutoka katika
kabila la Isakari, Kedeshi na
malisho yake, Daberathi^h na
malisho yake,ⁱ **73** Ramothi
na malisho yake, na Anemu
na malisho yake; **74** na kuto-
ka katika kabila la Asheri, Ma-
shali na malisho yake, Abdoni
na malisho yake,^j **75** Hukoki
na malisho yake, na Rehobu^k
na malisho yake; **76** na kuto-
ka katika kabila la Naftali, Ke-
deshi^l kule Galilaya^m na mali-
sho yake, Hamoni na malisho
yake, na Kiriathaimu na mali-
sho yake.

77 Wamerari waliobaki wa-
lipewa kutoka katika kabila la
Zabuloni,ⁿ Rimono na malisho
yake, Tabori na malisho yake;
78 na katika eneo la Yorda-
ni kule Yeriko, upande wa ma-
shariki wa Yordani, kutoka ka-
tika kabila la Rubeni, wali-
pewa Beseri kule nyikani na
malisho yake, Yahazi^o na mali-
sho yake, **79** Kedemothi^p na
malisho yake, na Mefaathi na

6:67 *Au labda, "jiji la," kulingana na
Yos 21:21.

malisho yake; **80** na kutoka katika kabila la Gadi, Ramothi kule Gileadi na malisho yake, Mahanaimu^a na malisho yake, **81** Heshboni^b na malisho yake, na Yazeri^c na malisho yake.

7 Sasa wana wa Isakari walikuwa Tola, Pua, Yashubu, na Shimroni^d—wana wanne. **2** Na wana wa Tola walikuwa Uzi, Refaya, Yerieli, Yahmai, Ibsamu, na Shemueli, viongozi wa koo* zao. Wazao wa Tola walikuwa mashujaa hodari, na idadi yao katika siku za Daudi ilikuwa 22,600. **3** Na wazao* wa Uzi walikuwa Izrahia na wana wa Izrahia: Mikaeli, Obadia, Yoeli, na Ishia—wote watano walikuwa wakuu.^e **4** Na pamoja nao, kulingana na wazao wao, kulingana na koo* zao, kulikuwa na wanajeshi 36,000 katika jeshi lao waliokuwa tayari kwa ajili ya vita, kwa maana walikuwa na wake wengi na wana wengi. **5** Na ndugu zao wa koo zote za Isakari walikuwa mashujaa hodari 87,000 walioandikishwa katika orodha ya koo.^e

6 Wana wa Benjamini^f walikuwa Bela,^g Bekeru,^h na Yediaeliⁱ—wana watatu. **7** Na wana wa Bela walikuwa Esboni, Uzi, Uzieli, Yerimothi, na Iri—wana watano—viongozi wa koo zao, mashujaa hodari, na 22,034 walikuwa wameandikishwa katika orodha ya ukoo* wao.^j **8** Na wana wa Bekeru walikuwa Zemira, Yoashi, Eliezeri, Elioenai, Omri, Yeremothi, Abiya, Anathothi, Alem-

7:2, 4, 7, 9 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 7:3, 13, 17 *Tnn., "wana." 7:3 "Tnn., "viongozi."

SURA YA 6

a Mwa 32:1, 2
2Sa 2:8

b Hes 21:26

c Hes 32:1

SURA YA 7

d Mwa 46:13
Hes 26:23, 24

e Hes 26:25

f Mwa 35:16, 18
Hes 26:38, 39

g 1Nya 8:1

h Mwa 46:21

i 1Nya 7:10

j Hes 26:41

Safu ya 2

a 1Nya 7:6

b 1Nya 7:7

c Hes 26:48, 49

d Mwa 30:3, 8
Mwa 46:24, 25

e Mwa 41:50, 51

f Mwa 50:23
Hes 26:29
Kum 3:15

g Hes 26:33

h Hes 27:1, 7

thi—hao wote walikuwa wana wa Bekeru. **9** Na wale walioandikishwa katika orodha ya ukoo wao kulingana na wazao wao kuhusiana na viongozi wa koo* zao walikuwa mashujaa hodari 20,200. **10** Na wana wa Yediaeli^a walikuwa Bilhani na wana wa Bilhani walikuwa Yeushi, Benjamini, Ehudi, Kenaana, Zethani, Tarshishi, na Ahishahari. **11** Hao wote walikuwa wana wa Yediaeli, kulingana na viongozi wa koo za mababu zao, mashujaa hodari 17,200 waliokuwa tayari kujiunga na jeshi kwa ajili ya vita.

12 Washupimu na Wahupimu walikuwa wana wa Ire;^b Wahushimu walikuwa wana wa Aheri.

13 Wana wa Naftali^c walikuwa Yahzieli, Guni, Yezeri, na Shalumu—wazao* wa Bilha.^d

14 Wana wa Manase^e Asrieli, aliyezaliwa na suria wake Msiria. (Suria huyo alimzaa Makiri^f baba ya Gileadi. **15** Makiri alimtafutia mke Hupimu na Shupimu, na dada yake alitwa Maaka.) Mwana wa pili alitwa Selofehadi, lakini Selofehadi^g alizaa mabinti.^h **16** Maaka, mke wa Makiri, alizaa mwana na kumwita jina Pereshi; na ndugu yake alitwa Shereshi; na wanawe walikuwa Ulamu na Rekemu. **17** Na mwana* wa Ulamu alikuwa Bedani. Hao ndio waliokuwa wana wa Gileadi mwana wa Makiri mwana wa Manase. **18** Na dada yake alikuwa Hamolekethi. Alimzaa Ishodi, Abiezeri, na Mala. **19** Na wana wa Shemida walikuwa Ahiani, Shekemu, Likhi, na Aniamu.

20 Wana wa Efraimu^a walikuwa Shuthela,^b Beredi mwana wa Shuthela, Tahathi mwana wa Beredi, Eleada mwana wa Tahathi, na Tahathi mwana wa Eleada, **21** Zabadi mwana wa Eleada, Shuthela mwana wa Zabadi, Ezeri, na Eleadi. Wanaume wa Gathi^c waliozaliwa nchini waliwaua kwa sababu waliteremka huko kuchukua mifugo yao. **22** Efraimu baba yao aliendelea kuomboleza kwa siku nyingi, na ndugu zake walikuwa wakija kumfariji. **23** Baadaye akalala na mke wake, naye akapata mimba na kuzaa mwana. Lakini akamwita mwana huyo Beria* kwa sababu mama yake alikuwa katika nyumba ya Efraimu wakati wa msiba. **24** Na binti yake alikuwa Sheera, aliyejenga Beth-horoni ya Chini^d na ya Juu^e na Uzen-sheera. **25** Na kulikuwa na Refa mwanawe, Reshefu, Tela mwana wa Reshefu, Tahani mwana wa Tela, **26** Ladani mwana wa Tahani, Amihudi mwana wa Ladani, Elishama mwana wa Amihudi, **27** Nuni mwana wa Elishama, na Yohua*^f mwana wa Nuni.

28 Walimiliki na kuishi Betheli^g na katika miji yake, na upande wa mashariki, Naarani, na upande wa magharibi, Gezeri na miji yake, na Shekemu* na miji yake, mpaka Aya na miji yake; **29** na kando ya wazao wa Manase, walimiliki Beth-sheani^h na miji yake, Taanakiⁱ na miji yake, Megido/

7:23 *Maana yake "Wakati wa Msiba." 7:27 *Au "Yehoshua," linalomaanisha "Yehova Ni Wokovu." 7:28 *Au labda, "Gaza," ingawa si jiji la Gaza kule Ufilisti.

SURA YA 7

a Hes 1:33

b Hes 26:35

c 1Sa 7:14
1Sa 17:4

d Yos 16:1,3

e Yos 16:5
Yos 21:20, 22
2Nya 8:3, 5f Kut 33:11
Hes 11:28
Hes 32:11, 12
Kum 34:9
Yos 1:1g Mwa 28:16, 19
Yos 16:1, 2h Yos 17:11
1Sa 31:8, 10

i Amu 5:1, 19

j Amu 1:27
1Fa 9:15

Safu ya 2

a 1Fa 4:7, 11

b Hes 26:44, 45

c Mwa 46:17

d Kut 30:14

e Hes 1:41
Hes 26:47

SURA YA 8

f Mwa 35:16, 18

g 1Nya 7:6

h Mwa 46:21

i Mwa 46:21

na miji yake, na Dori^a na miji yake. Wazao wa Yosefu mwana wa Israeli waliishi humo.

30 Wana wa Asheri walikuwa Imna, Ishva, Ishvi, na Beria,^b na dada yao alitwa Sera.^c **31** Wana wa Beria walikuwa Heberi na Malkieli, aliyekuwa baba ya Birzaithi. **32** Heberi akamzaa Yafleti, Shomeri, na Hothamu, na Shua dada yao. **33** Wana wa Yafleti walikuwa Pasaki, Bimhali, na Ashvathi. Hao ndio waliokuwa wana wa Yafleti. **34** Wana wa Shemeri* walikuwa Ahi, Roga, Yehuba, na Aramu. **35** Wana wa Helemu* ndugu yake walikuwa Sofa, Imna, Sheleshi, na Amali. **36** Wana wa Sofa walikuwa Sua, Harneferi, Shuali, Beri, Imra, **37** Beseri, Hodi, Shama, Shilsha, Ithrani, na Beera. **38** Wana wa Yetheri walikuwa Yefune, Pispa, na Ara. **39** Wana wa Ula walikuwa Ara, Hanieli, na Risia. **40** Hao wote walikuwa wana wa Asheri, viongozi wa koo* zao, watu wa pekee, mashujaa hodari, viongozi wa wakuu; na wanaume wao walioandikishwa jeshini kwa ajili ya vita katika orodha ya koo^d walikuwa 26,000.^e

8 Benjamini^f alimzaa Bela^g mzaliwa wake wa kwanza, wa pili Ashbeli,^h wa tatu Ahara, **2** wa nne Noha, na wa tano Rafa. **3** Wana wa Bela walikuwa Adari, Gera,ⁱ Abihudi, **4** Abishua, Naamani, Ahoa, **5** Gera, Shefufani, na Huramu. **6** Hawa walikuwa wana wa Ehudi, viongozi wa

7:34 *Pia anaitwa Shomeri katika mstari wa 32. 7:35 *Inaelekea ni sawa na "Hothamu" katika mstari wa 32. 7:40 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

koo* za wakaaji wa Geba,^a waliopelekwa uhamishoni kule Manahathi: **7** Naamani, Ahia, na Gera—ndiye aliyewapeleka uhamishoni, naye alimzaa Uza na Ahihudi. **8** Shahraraimu aliwazaa watoto katika eneo* la Moabu baada ya kuwafukuza Wamoabu. Wake zake walikuwa Hushimu na Baara.[#] **9** Na kupitia Hodeshi mke wake, alimzaa Yobabu, Sibia, Meshu, Malkamu, **10** Yeuzi, Sakia, na Mirma. Hao walikuwa wanawe, viongozi wa koo.*

11 Na kupitia Hushimu alimzaa Abitubu na Elpaali. **12** Na wana wa Elpaali walikuwa Eberi, Mishamu, Shemedi (aliyejenga Ono^b na Lodi^c pamoja na miji yake), **13** Beria, na Shema. Hao walikuwa viongozi wa koo* za wakaaji wa Aiyaloni.^d Hao ndio waliowafukuza wakaaji wa Gathi. **14** Na kulikuwa na Ahio, Shashaki, Yeremothi, **15** Zebadia, Aradi, Ederi, **16** Mikaeli, Ishpa, Yoha, wana wa Beria; **17** na Zebadia, Meshulamu, Hizki, Heberi, **18** Ishmerai, Izlia, Yobabu, wana wa Elpaali; **19** na Yakimu, Zikri, Zabdi, **20** Elienai, Zilethai, Elieli, **21** Adaya, Beraya, Shmrathi, wana wa Shimeji; **22** na Ishpani, Eberi, Elieli, **23** Abdoni, Zikri, Hanani, **24** Hanania, Elamu, Anthothiya, **25** Ifdeya, Penueli, wana wa Shashaki; **26** na Shamsherai, Sheharia, Athalia, **27** Yareshia, Eliya, Zikri, wana wa Yerohamu. **28** Hao walikuwa viongozi wa koo*

8:6, 10, 13, 28 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. **8:8** *Tnn., "shamba." [#]Au labda, "baada ya kuwafukuza wake zake Hushimu na Baara."

SURA YA 8

a Yos 21:8, 17
1Sa 13:16

b Ne 6:2

c Ezz 2:1, 33

d Yos 19:42, 48
Yos 21:8, 24

Safu ya 2

a Yos 9:15, 17
Yos 21:8, 17
1Nya 21:29

b 1Nya 9:35-38

c 1Sa 14:50

d 1Sa 9:1, 2
1Sa 11:15

e 1Sa 14:45

f 1Sa 14:49

g 1Sa 31:2

h 2Sa 2:8
1Nya 9:39-44

i 2Sa 4:4

j 2Sa 9:12

zao kulingana na wazao wao. Viongozi hao waliishi Yerusalemu.

29 Yeieli, baba ya Gibeoni, aliishi Gibeoni.^a Mke wake alii-twa Maaka.^b **30** Na mwana wake mzaliwa na kwanza alikuwa Abdoni, kisha Suri, Kishi, Baali, Nadabu, **31** Gedori, Ahio, na Zekeri. **32** Miklothi alimzaa Shimea. Na wote waliishi karibu na ndugu zao kule Yerusalemu, pamoja na ndugu zao wengine.

33 Neri^c alimzaa Kishi; Kishi akamzaa Sauli;^d Sauli akamzaa Yonathani,^e Malki-shua,^f Abinadabu,^g na Eshbaali.^{*h}

34 Na mwana wa Yonathani alii-twa Merib-baali.^{*i} Merib-baali akamzaa Mika.^j **35** Na wana wa Mika walikuwa Pithoni, Meleki, Tarea, na Ahazi. **36** Ahazi akamzaa Yehoda; Yehoda akamzaa Alemethi, Azmavethi, na Zimri. Zimri akamzaa Mosa. **37** Mosa akamzaa Binea, Binea akamzaa Rafa, Rafa akamzaa Eleasa, Eleasa akamzaa Aseli. **38** Aseli alikuwa na wana sita, na haya ndiyo majina yao: Azrikamu, Bokeru, Ishmaeli, Shearia, Obadia, na Hanani. Hao wote ndio waliokuwa wana wa Aseli. **39** Na wana wa Esheki ndugu yake walikuwa Ulamu mzaliwa wake wa kwanza, wa pili Yeushi, na wa tatu Elifeleti. **40** Na wana wa Ulamu walikuwa mashujaa hodari walioweza kushika* upinde, nao walikuwa na wana wengi na wajukuu wengi, jumla yao 150. Hao wote walikuwa wazao wa Benjamini.

8:33 *Pia alii-twa Ish-boshethi. **8:34** *Pia alii-twa Mefiboshethi. **8:40** *Tnn., "kukanyaga."

9 Waisraeli wote waliandikishwa kulingana na ukoo wao, na koo hizo zimeandikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Israeli. Na watu wa Yuda walipeleka uhamishoni kule Babiloni kwa sababu hawakuwa waaminifu.^a **2** Baadhi ya Waisraeli, makuhani, Walawi, na watumishi wa hekaluni*^b walikuwa wakaaji wa kwanza kurudi katika miliki yao kwenye majiji yao. **3** Na baadhi ya wazao wa Yuda,^c wa Benjamini,^d wa Efraimu, na wa Manase walioishi Yerusalem walikuwa: **4** Uthai mwana wa Amihudi mwana wa Omri mwana wa Imri mwana wa Bani, kutoka kwa wazao wa Perezi^e mwana wa Yuda. **5** Na kutoka kwa wazao wa Washilo, Asaya mzaliwa wa kwanza na wanawe. **6** Na wana wa Zera,^f Yeueli na ndugu zao 690.

7 Na kutoka kwa wazao wa Benjamini, Salu mwana wa Meshulamu mwana wa Hodavia mwana wa Hasenua, **8** Ibneya mwana wa Yerohamu, Ela mwana wa Uzi mwana wa Mikri, na Meshulamu mwana wa Shefatia mwana wa Reueli mwana wa Ibniya. **9** Na ndugu zao kulingana na ukoo wao walikuwa 956. Wanaume hao wote walikuwa viongozi wa koo zao.*

10 Na kutoka kwa makuhanini, kulikuwa na Yedaya, Yehoyaribu, Yakini,^g **11** Azaria mwana wa Hilkia mwana wa Meshulamu mwana wa Sadoiki mwana wa Merayothi mwana wa Ahitubu, kiongozi wa

9:2 *Au "Wanethini." Tnn., "waliotolewa." 9:9 *Tnn., "vichwa vya akina baba kwa ajili ya nyumba za baba zao."

SURA YA 9

a Yer 39:9

b Yos 9:3, 27
Ezr 2:43-54
Ezr 2:70
Ezr 8:20
Ne 7:73
Ne 11:3

c Ne 11:4, 5

d Ne 11:7-9

e Mwa 46:12
1Nya 2:4

f 1Nya 2:4, 6

g Ne 11:10-14

Safu ya 2

a Ne 11:15

b 1Nya 2:54
Ne 12:28c Ezr 2:1, 42
Ne 11:19

d Ne 3:29

e Hes 25:11, 13
Yos 22:30
Amu 20:28f Kut 6:25
Hes 3:32

nyumba ya* Mungu wa kweli, **12** Adaya mwana wa Yerohamu mwana wa Pashuri mwana wa Malkiya, Maasai mwana wa Adieli mwana wa Yahzera mwana wa Meshulam mwana wa Meshilemithi mwana wa Imeri, **13** na ndugu zao, viongozi wa koo* zao, mashujaa 1,760, wanaume wenye uwezo waliokuwa tayari kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya Mungu wa kweli.

14 Na kutoka kwa Walawi, kulikuwa na Shemaya^a mwana wa Hashubu mwana wa Azrikamu mwana wa Hashabia kutoka kwa wazao wa Merari; **15** na Bakbakari, Hershish, Galali, Matania mwana wa Mika mwana wa Zikri mwana wa Asafu, **16** Obadia mwana wa Shemaya mwana wa Galali mwana wa Yeduthuni, na Berekia mwana wa Asa mwana wa Elkana, aliyekuwa akiishi katika vijiji vya Wanetofa.^b

17 Walinzi wa malango^c walikuwa Shalumu, Akubu, Talmoni, Ahimani, na ndugu yao Shalumu alikuwa kiongozi, **18** na kufikia wakati huo alikuwa katika lango la mfalme upande wa mashariki.^d Hao walikuwa walinzi wa malango wa kambi za Walawi. **19** Na Shalumu mwana wa Kore mwana wa Ebiasafu mwana wa Kora, na ndugu zake wa ukoo wake,* Wakora, walisimamia majukumu ya utumishi wa walinzi wa milango ya hema, na baba zao walikuwa wakisimamia kambi ya Yehova wakiwa walinzi wa njia ya kuingilia. **20** Finehasi^e mwana wa Eleazari^f ndi-

9:11 *Au "hekalu la." 9:13, 19 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

ye aliyekuwa kiongozi wao zamani; Yehova alikuwa pamoja naye. **21** Zekaria^a mwana wa Meshelemia alikuwa mlinzi wa lango la kuingia katika hema la mkutano.

22 Wote waliochaguliwa kuwa walenzi kwenye vizingiti walikuwa 212. Waliishi katika vijiji vyao kulingana na orodha ya ukoo wao.^b Daudi na Samweli yule mwonaji^c waliwaka katika wadhifa wa kuaminiwa. **23** Watu hao pamoja na wana wao walisimamia utumishi wa ulinzi wa malango ya nyumba ya Yehova,^d nyumba ya hema. **24** Walenzi wa malango walikuwa pande zote nne—mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini.^e **25** Mara kwa mara, ndugu zao walipaswa kuja kwa siku saba kutoka katika vijiji vyao ili kutumikia pamoja nao. **26** Kulikuwa na walenzi wakuu* wanne waliowe kwa katika wadhifa huo wa kuaminiwa. Walikuwa Walawi, nao walisimamia vyumba^f na hazina za nyumba ya Mungu wa kweli.^f **27** Walikuwa wakikeshwa usiku kucha katika vituo vyao kuzunguka nyumba yote ya Mungu wa kweli, kwa maana walishughulikia utumishi wa ulinzi na kutunza ufunguo, nao walikuwa wakifungua nyumba hiyo asubuhi baada ya asubuhi.

28 Baadhi yao walisimamia vyombo^g vya utumishi; walikuwa wakivihesabu vilipokuwa vikiingizwa ndani na kuvihesabu vilipotolewa nje. **29** Baadhi yao waliwekwa kusimamia vyombo, kusimamia

9:26 *Tnn., "wenye uwezo." 9:26, 33
^fAu "vyumba vya kulia chakula."

SURA YA 9

a 1Nya 26:14, 19

b 1Nya 9:1

c 1Sa 9:9

d 2Nya 23:16, 19
Ne 12:45

e 1Nya 26:14-16

f 1Nya 26:20
1Nya 28:11, 12
2Nya 31:12

g Hes 1:50

Safu ya 2

a 1Fa 8:4

b Law 2:1
1Nya 23:29

c Law 23:12, 13

d Kut 27:20

e Law 2:1, 2

f Kut 25:3, 6

g Law 2:5, 7

h 2Nya 2:4
2Nya 13:11

i Law 24:6, 8

j Yos 21:8, 17

k 1Sa 14:50

l 1Sa 9:1, 2
1Sa 11:15m 1Sa 14:45
1Sa 18:1
2Sa 1:23

n 1Sa 14:49

o 1Sa 31:2

p 2Sa 4:4

q 2Sa 9:12

vyombo vyote vitakatifu,^a na kusimamia unga laini,^b divai,^c mafuta,^d ubani,^e na mafuta ya zeri.^f **30** Baadhi ya wana wa makuhani walichanganya manukoto ya mafuta ya zeri. **31** Na Matithia mmoja wa Walawi, aliyekuwa mzaliwa wa kwanza wa Shalumu, Mkora, alipewa wadhifa wa kuaminiwa wa kusimamia vitu vilivyookwa kwenye vikaangio.^g **32** Baadhi ya ndugu zao Wakohathi walisimamia mikate ya tabaka,^h waliitayarisha kila sabato.ⁱ

33 Hao walikuwa waimbaji, kiongozi wa koo* za Walawi katika vyumba^j vya nyumba hiyo, wale ambao hawakupewa kazi nyingine; kwa maana usiku na mchana walikuwa na wajibu wa kushika zamu zao. **34** Hao walikuwa viongozi wa koo* za Walawi kulingana na ukoo wao, viongozi. Waliishi Yerusalemu.

35 Yeieli, baba ya Gibeoni, aliishi Gibeoni.^j Mke wake alitwa Maaka. **36** Na mwana wake mzaliwa wa kwanza alitwa Abdoni, kisha Suri, Kishi, Baali, Neri, Nadabu, **37** Gedori, Ahio, Zekaria, na Miklothi. **38** Miklothi alimzaa Shimeamu. Na wote waliishi karibu na ndugu zao kule Yerusalemu, pamoja na ndugu zao wengine. **39** Neri^k akamzaa Kishi; Kishi akamzaa Sauli;^l Sauli akamzaa Yonathani,^m Malki-shua,ⁿ Abinadabu,^o na Eshbaali. **40** Na mwana wa Yonathani alitwa Meribbaali.^p Meribbaali akamzaa Mika.^q **41** Na wana wa Mika walikuwa Pithoni, Meleki,

9:32 *Yaani, mikate ya wonyesho.
 9:33, 34 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

Tahrea, na Ahazi. **42** Ahazi akamzaa Yara; Yara akamzaa Alemethi, Azmavethi, na Zimri. Zimri akamzaa Mosa. **43** Mosa akamzaa Binea na Refaya mwanawe, Refaya akamzaa Eleasa, Eleasa akamzaa Aseli. **44** Aseli alikuwa na wana sita, na haya ndiyo majina yao: Azrikamu, Bokeru, Ishmaeli, Shearia, Obadia, na Hanani. Hao ndio waliokuwa wana wa Aseli.

10 Sasa Wafilisti walikuwa wakipigana na Waisraeli. Na wanaume wa Israeli wakawakimbia Wafilisti, na wengi wakauawa kwenye Mlima Gilboa.^a **2** Wafilisti wakamkaribia sana Sauli na wanawe, nao wakamuua Yonathani, Abinadabu, na Malki-shua,^b wana wa Sauli. **3** Vita vikawa vikali sana dhidi ya Sauli, na wapiga mishale wakampata na kumjeruhi.^c **4** Ndipo Sauli akamwambia mtu aliyembebea silaha: "Chomoa upanga wako unichome nao, ili watu hawa wasiotahiriwa wasije kunitendea kikatili."^{*d} Lakini mtu aliyembebea silaha hakutaka kufanya hivyo, kwa sababu alio-gopa sana. Basi Sauli akachukua upanga na kuuangukia.^e **5** Mtu aliyembebea silaha alipoona kwamba Sauli amekufa, yeye pia akauangukia upanga wake mwenyewe na kufa. **6** Basi Sauli na wanawe watatu wakafa, na watu wote wa nyumba yake wakafa pamoja.^f **7** Watu wote wa Israeli waliokuwa bondeni* walipoona kwamba kila mtu amekimbia na kwamba Sauli na wanawe

10:4 *Au "wasije kunitesa." 10:7 *Au "katika nchi tambarare ya chini."

SURA YA 10

a 1Sa 31:1-5
2Sa 1:21, 25

b 1Nya 8:33

c 1Sa 26:9, 10

d Amu 16:21, 23

e 1Nya 10:13

f 1Sa 31:6, 7

Safu ya 2

a 1Sa 28:4
1Sa 31:8-10

b Amu 16:23, 24

c 1Sa 5:2

d 1Sa 11:1

e 1Sa 31:11-13

f 2Sa 2:5
2Sa 21:12

g 1Sa 13:13
1Sa 15:22, 23

h Law 20:6
1Sa 28:7

i Ru 4:17
1Sa 13:14
1Sa 15:27, 28
2Sa 5:3

SURA YA 11

j Hes 13:22
2Sa 2:1
2Sa 5:5
1Nya 12:23

k 2Sa 5:1, 2

wamekufa, wakaanza kuyaa-cha majiji yao na kukimbia; kisha Wafilisti wakaja na kuka humo.

8 Siku iliyofuata, Wafilisti walipokuja kuwawua waliouwa vitu walivyokuwa navyo, walimkuta Sauli na wanawe wakiwa wameanguka kwenye Mlima Gilboa.^a **9** Basi wakamvua mavazi yake, wakamkata kichwa na kuchukua silaha zake, nao wakatuma ujumbe kotekote katika nchi ya Wafilisti ili habari hizo zienezwe kwa sanamu^b zao na watu. **10** Kisha wakaweka silaha zake katika nyumba ya* mungu wao na kulitundika fuvu lake kwenye nyumba ya Dagoni.^c

11 Wakaaji wote wa Yabeshi^d kule Gileadi waliposikia mambo yote ambayo Wafilisti walikuwa wamemtendea Sauli,^e **12** mashujaa wote wakaondoka na kubeba maiti ya Sauli na maiti za wanawe. Wakawaleta Yabeshi na kuzika mifupa yao chini ya mti mkubwa kule Yabeshi,^f nao wakafunga kwa siku saba.

13 Kwa hiyo Sauli alikufa kwa sababu hakuwa mwaminifu kwa Yehova, ^g na pia kwa sababu alitafuta ushauri kutoka kwa mtu aliyewasiliana na roho^h **14** badala ya kutafuta ushauri kutoka kwa Yehova. Kwa hiyo Akamuua na kumpa Daudi mwana wa Yese ufalme.ⁱ

11 Baada ya muda Waisraeli wote wakakusanika kwa Daudi kule Hebroni/ na kusema: "Tazama! Sisi ni mfupa wako na nyama yako."^{*k}

10:10 *Au "hekalu la." 11:1 *Tnn., "Tuna uhusiano wa damu nawe."

2 Zamani, Sauli alipokuwa mfalme, ni wewe uliyewaongoza Waisraeli vitani.*^a Na Yehova Mungu wako alikuambia hivi: 'Utawachunga watu wangu Waisraeli, nawe utakuwa kiongozi wa watu wangu Waisraeli.'"^b **3** Basi wazee wote wa Israeli wakaja kwa mfalme huko Hebroni, na Daudi akafanya agano nao huko Hebroni mbele za Yehova. Kisha wakamtia mafuta Daudi awe mfalme wa Israeli,^c kulingana na neno la Yehova kupitia Samweli.^d

4 Baadaye Daudi na Waisraeli wote wakaenda Yerusalemu, yaani, Yebusi,^e ambako Wayebusi^f walikuwa wakiiishi. **5** Wakaaji wa Yebusi walimdhihakiki Daudi wakisema: "Hutaingia humu kamwe!"^g Hata hivyo, Daudi aliitaka ngome ya Sayuni,^h ambayo sasa ni Jiji la Daudi.ⁱ **6** Kwa hiyo Daudi akasema: "Yeyote atakayekuwa wa kwanza kuwashambulia Wayebusi atakuwa kiongozi* na mkuu." Basi Yoabu/^j mwana wa Seruya akawa wa kwanza kupanda huko kuwashambulia, akawa kiongozi. **7** Kisha Daudi akaanza kukaa katika ngome hiyo. Ndiyo sababu waliita Jiji la Daudi. **8** Akaanza kujenga jiji hilo pande zote, kuanzia kwenye Kilima* mpaka kwenye maeneo yanayozunguka, na Yoabu akajenga upya sehemu zilizobaki za jiji hilo. **9** Kwa hiyo Daudi akawa mkuu zaidi na zaidi,^k na Yehova wa majeshi alikuwa pamoja naye.

11:2 *Tnn., "uliyekuwa ukiwatoa nje na kuwaingiza ndani Waisraeli." 11:6 *Tnn., "kichwa." 11:8 *Au "Milo." Neno la Kiebrania linalomaanisha "jaza."

SURA YA 11

a 1Sa 18:6,13

b 2Sa 6:21
2Sa 7:8,9
Zb 78:70,71c 1Sa 16:13
2Sa 2:4
2Sa 5:3

d 1Sa 15:27,28

e Yos 15:63
Amu 1:21
Amu 19:10f Mwa 10:15,16
Mwa 15:18,21
Kut 3:17

g 2Sa 5:6-10

h 1Fa 8:1
Zb 2:6
Zb 48:2

i 1Fa 2:10

j 2Sa 2:18

k 2Sa 3:1

Safu ya 2

a 1Sa 16:12,13

b 1Nya 27:1,2

c 2Sa 23:8

d Yos 23:10

e 2Sa 23:9,10
2Sa 23:15-17

f 1Nya 8:1,4

g 1Sa 17:1

h Zb 18:50

i 1Sa 22:1

j Yos 15:8,12
2Sa 23:13-17

k 1Sa 20:6

10 Sasa hawa ndio viongozi wa mashujaa hodari wa Daudi, waliomuunga mkono kwa dhati katika utawala wake, pamoja na Waisraeli wote, ili wamweke kuwa mfalme kulingana na neno alilosema Yehova kuhusu Israeli.^a **11** Hii ndiyo orodha ya mashujaa hodari wa Daudi: Yashobeamu^b mwana wa Mhakmoni, kiongozi wa wale watatu.^c Wakati mmoja, alitumia mkuki wake kuwaua watu 300.^d **12** Aliyemfuata ni Eleazari^e mwana wa Dodo mwana wa Aho-hi.^f Alikuwa miongoni mwa mashujaa hao watatu hodari. **13** Alikuwa na Daudi kule Pas-damimu,^g ambako Wafilisti walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya vita. Basi palikuwa na shamba lililojaa shayiri, na watu walikuwa wamekimbua kwa sababu ya Wafilisti. **14** Lakini alisimama katikati ya shamba hilo na kuwazuia Wafilisti wasiingie humo, naye aliendelea kuwaua Wafilisti, hivi kwamba Yehova akawapa ushindi* mkubwa.^h

15 Viongozi watatu kati ya wale viongozi 30 walishuka mwambani kwa Daudi, katika pango la Adulamu,ⁱ wakati jeshi la Wafilisti lilipokuwa limepiga kambi katika Bonde la* Refaimu.^j **16** Wakati huo Daudi alikuwa ndani ya ngome, na kikosi cha wanajeshi Wafilisti kilikuwa Bethlehemu. **17** Kisha Daudi akasema alichotamani: "Laiti ninge kunywa maji kutoka katika tangi lililo karibu na lango la Bethlehemu!"^k **18** Ndipo wale mashujaa watatu wa-kaingia kwa nguvu katika

11:14 *Au "wokovu." 11:15 *Au "Nchi Tamarare ya Chini ya."

kambi ya Wafilisti, wakateka maji kutoka katika tangi hilo lililo karibu na lango la Bethlehemu na kumletea Daudi; lakini Daudi akakataa kuyanywa, akayamwaga mbele za Yehova. **19** Akasema: “Ni jambo nililoweza kamwe kuwazia, kulingana na maoni ya Mungu wangu, kufanya hivyo! Je, ninywe damu ya wanauwe hawa waliohatarisha uhai wao?”*^a Kwa maana waliohatarisha uhai wao kwenda kuyaleta. Basi akakataa kuyanywa. Hayo ndiyo mambo waliyotenda mashujaa wake watatu hodari.

20 Abishai^b ndugu ya Yoabu^c akawa kiongozi wa wengine watatu; alitumia mkuki wake kuwaua watu 300, naye alikuwa maarufu kama wale watatu.^d **21** Ingawa alikuwa mashuhuri zaidi kuliko wale wengine watatu, na alikuwa kiongozi wao, hakuwa shujaa kama wale watatu wa kwanza.

22 Benaya^e mwana wa Yehoyada alikuwa mwanamume jasiri* aliyefanya mambo mengi ya kishujaa kule Kabzeeli.^f Aliwaua wana wawili wa Arieli wa Moabu, naye aliingia ndani ya shimo la maji siku ya theluji na kumuua simba.^g

23 Alimuua pia mwanamume Mmisri aliyekuwa mkubwa isivyo kawaida—mwenye urefu wa mikono mitano.*^h Ingawa Mmisri huyo alikuwa na mkuki mkononi kama mti wa wafumaji wa nguo,ⁱ Benaya alikabili naye akiwa na fimbo, akamnyang’anya Mmisri huyo mkuki kutoka

11:19 *Au “nafsi zao.” 11:22 *Tnn., “mwana wa mwanamume jasiri.” 11:23 *Urefu wake ulikuwa karibu mita 2.23 (futi 7.3). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 11

a Mwa 9:4
Law 17:10

b 1Sa 26:6
2Sa 2:18
2Sa 18:2

c 2Sa 3:30

d 2Sa 23:18, 19

e 1Fa 4:4
1Nya 27:1, 5

f Yos 15:21

g Amu 14:5, 6
1Sa 17:36, 37
2Sa 23:20-23

h 1Sa 17:4

i 1Sa 17:7

Safu ya 2

a 1Sa 17:51

b 1Nya 11:19

c 2Sa 2:18, 23
1Nya 27:1, 7

d 2Sa 23:24-39

e 1Nya 27:1, 9

f 1Nya 27:1, 12

g 2Sa 21:18
1Nya 27:1, 11

h 1Nya 27:1, 13

i 1Nya 27:1, 15

j Amu 20:15
1Nya 12:1, 2

k Yos 24:30

l 2Sa 11:3, 17
2Sa 12:9
1Fa 15:5

mkononi mwake na kumuua kwa mkuki wake mwenyewe.^a

24 Benaya mwana wa Yehoyada alifanya mambo hayo, naye alikuwa maarufu kama wale mashujaa watatu hodari.

25 Ingawa alikuwa mashuhuri hata kuliko wale 30, hakuwa shujaa kama wale watatu.^b Lakini Daudi alimweka kuwa kiongozi wa walinzi wake binafsi.

26 Mashujaa hodari jeshini walikuwa Asaheli^c ndugu ya Yoabu, Elhanani mwana wa Dodo wa Bethlehemu,^d

27 Shamothi Mharori, Helezi Mpeloni, **28** Ira^e mwana wa Ikeshi Mtekoa, Abiezeri^f Mwanathothi, **29** Sibekai^g Mhusha, Ilai Mwahohi, **30** Maharai^h Mnetofa, Helediⁱ mwana wa Baana Mnetofa, **31** Ithai mwana wa Ribai wa jiji la Gibea la Wabenjamini,^j Benaya Mpirathoni, **32** Hurai kutoka katika makorongo* ya Gaashi,^k Abieli Mwarbathi,

33 Azmavethi Mbaharumu, Eliaba Mshaalboni, **34** wana wa Hashemu Mgizoni, Yonathani mwana wa Shagee Mharari, **35** Ahiamu mwana wa Sakari Mharari, Elifali mwana wa Uru, **36** Heferi Mmekerathi, Ahiya Mpeloni, **37** Hezro Mkarmeli, Naarai mwana wa Ezbai, **38** Yoeli ndugu wa Nathani, Mibhari mwana wa Hagri, **39** Seleki Mwamoni, Naharai Mberothi, aliyembebea silaha Yoabu mwana wa Seruya; **40** Ira Mwithri, Garebu Mwithri,

41 Uria^l Mhiti, Zabadi mwana wa Alai, **42** Adina mwana wa Shiza Mrubeni, kiongozi wa Warubeni, aliyekuwa na watu 30; **43** Hanani mwana

11:32 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

wa Maaka, Yoshafati Mmithini, **44** Uziya Mwashtarothi, Shama na Yeieli, wana wa Hothamu Mwaroeri; **45** Yediaeli mwana wa Shimri, na Yohandugu yake, Mtisi; **46** Elieli Mmahawi, Yeribai na Yoshavia wana wa Elnaamu, na Ithma Mmoabu; **47** Elieli, Obedi, na Yaasieli Mmesoba.

12 Hao ndio wanaume walioenda kumwona Daudi kule Siklagi^a wakati ambapo hakuwa na uhuru wa kute-mbea popote kwa sababu ya Sauli^b mwana wa Kishi, nao walikuwa miongoni mwa mashujaa hodari waliomuunga mkono vitani.^c **2** Walijihami kwa upinde, nao waliweza kutumia mkono wa kulia na kono wa kushoto^d kurusha mawe kwa kombeo^e au kupiga mishale kwa upinde. Walikuwa wazao wa ndugu za Sauli, kutoka Benjamini.^f **3** Kiongozi wao alikuwa Ahiezeri, pamoja na Yoashi, wote wawili walikuwa wana wa Shema Mgi-bea;^g Yezieli na Peleti wana wa Azmavethi,^h Baraka, Yehu Mwanathothi, **4** Ishmaya Mgibeoni,ⁱ shujaa hodari miongoni mwa wale 30^j na kiongozi wa wale 30; pia Yeria, Yahazieli, Yohanani, Yozabadi Mgedera, **5** Eluzai, Yerimothi, Bealia, Shemaria, Shefatia Mharifu, **6** Elkana, Ishia, Azareli, Yoezeri, na Yashobeamu, Wakora;^k **7** na Yoela na Zebadia wana wa Yerohamu wa Gedori.

8 Baadhi ya Wagadi walionda kujiunga na Daudi katika ngome kule nyikani;^l walikuwa mashujaa hodari, wana-jeshi waliozoezwa kwa ajili ya vita, waliosimama tayari wa-

SURA YA 12

a 1Sa 27:5, 6
2Sa 1:1

b 1Sa 27:1

c 1Nya 11:10

d Amu 3:15
Amu 20:15, 16

e 1Sa 17:49

f Mwa 49:27

g 1Sa 11:4

h 1Nya 11:26, 33

i Yos 9:3

j 1Nya 11:15

k Hes 26:10, 11

l 1Sa 23:14, 29
1Sa 24:22
1Nya 11:16

Safu ya 2

a Mwa 49:19
Kum 33:20

b Law 26:8

c 1Sa 22:1
1Sa 23:14
1Sa 24:22d 1Sa 24:12, 15
1Sa 26:23
Zb 7:6e Amu 6:34
Amu 13:24, 25

f 2Sa 15:21

kiwa na ngao kubwa na mku-ki, nao walikuwa na nyuso kama za simba na walikimbia mbio sana* kama swala mili-mani. **9** Ezeri ndiye aliyekuwa kiongozi wao, wa pili Obadia, wa tatu Eliabu, **10** wa nne Mishmana, wa tano Yeria, **11** wa sita Atai, wa saba Elieli, **12** wa nane Yohanani, wa tisa Elzabadi, **13** wa kumi Yeria, wa kumi na moja Makbanai. **14** Hao walikuwa wazao wa Gadi,^a viongozi wa jeshi. Mwenye uwezo mdogo zaidi angeweza kuwashinda watu 100, na mwenye uwezo mkubwa zaidi angeweza kuwashinda watu 1,000.^b **15** Hao ndio wanaume walio-vuka Yordani katika mwezi wa kwanza wakati kingo za mto huo zilipokuwa zimefurika, nao waliwafukuza watu wote waliokuwa wakiishi mabonde-ni, upande wa mashariki na wa magharibi.

16 Baadhi ya wanaume wa Benjamini na Yuda walikuja pia kwa Daudi katika ngome yake.^c **17** Kisha Daudi akatoka na kuwaambia: “Ikiwa mmekuja kwangu kwa amani ili kunisaidia, moyo wangu utaungana nanyi. Lakini ikiwa mmekuja kunisaliti kwa maadui wangu wakati mikono yangu haijatenda kosa lolote, Mungu wa mababu zetu na aone hilo na kuhukumu.”^d **18** Kisha roho ikamjia* Amasai,^e kiongozi wa wale 30, akasema:

“Sisi ni wako, Ee Daudi,
nasi tuko pamoja nawe,
Ee mwana wa Yese.^f

Amani, amani iwe yako, na

12:8 *Au “walikuwa wepesi.” **12:18**
*Tnn., “ikamvaa.”

amani iwe na yule anayekusaidia,

Kwa maana Mungu wako anakusaidia.”^a

Basi Daudi akawakaribisha na kuwaweka wawe miongoni mwa viongozi wa wanajeshi.

19 Baadhi ya watu wa kabila la Manase walitoroka pia na kujiunga na Daudi alipokuja pamoja na Wafilisti kupigana na Sauli; lakini hakuwasaidia Wafilisti, kwa sababu baada ya watawala wa Wafilisti^b kushauriana, walimfukuza wakisema: “Atatoroka na kwenenda kwa Sauli bwana wake, na jambo hilo litahatarisha vichwa vyetu.”^c **20** Alipoenda Siklagi,^d watu hawa wa kabila la Manase walitoroka na kujiunga naye: Adna, Yozabadi, Yediaeli, Mikaeli, Yozabadi, Elihu, na Zilethai, viongozi wa maelfu katika kabila la Manase.^e **21** Walimsaidia Daudi kupigana na kundi la wavamizi, kwa sababu wote walikuwa wanaume hodari walio jasiri,^f nao wakawa wakuu katika jeshi lake. **22** Siku baada ya siku watu waliendelea kuja kumsaidia Daudi^g mpaka kambi yake ikawa kubwa kama kambi ya Mungu.^h

23 Hii ndiyo idadi ya viongozi wa wale waliojihami kwa ajili ya vita ambao walijiunga na Daudi kule Hebronⁱ ili kumpa utawala wa Sauli kulingana na agizo la Yehova. **24** Wanaume wa Yuda waliolebeba ngao kubwa na mkuki walikuwa 6,800, waliojihami kwa ajili ya vita. **25** Kutoka kwa Wasimeoni, kulikuwa na wanajeshi 7,100, wanaume jasiri na hodari.

26 Kutoka kwa Walawi, 4,600. **27** Yehoyada^k alikuwa

SURA YA 12

a Zb 54:4

b Amu 3:1,3

c 1Sa 29:2-4

d 1Sa 30:1

e Kum 33:17

f 1Nya 5:23, 24
1Nya 11:10

g 2Sa 2:3

h 2Sa 3:1

i 2Sa 2:1
2Sa 5:1

j 1Sa 16:1,13
1Nya 11:10

k 1Nya 27:1, 5

Safu ya 2

a 1Nya 6:49

b 2Sa 8:17
1Fa 1:8
1Fa 2:35
1Nya 6:1, 8
1Nya 27:16, 17

c 1Nya 8:1, 33
1Nya 12:1, 2

d Hes 32:33
Yos 13:8

kiongozi wa wana wa Haruni,^a naye alikuwa pamoja na watu 3,700, **28** na pia Sadoki,^b kijana aliyekuwa hodari na jasiri, pamoja na wakuu 22 kutoka katika ukoo wake.*

29 Kutoka kwa Wabenjamine, ndugu za Sauli,^c kulikuwa na wanaume 3,000, ambao wengi wao, hapo awali, walikuwa wakilinda masilahi ya nyumba ya Sauli. **30** Kutoka kwa Waefraimu, kulikuwa na wanaume hodari 20,800, waliokuwa jasiri na maarufu katika koo zao.*

31 Na kutoka kwa nusu ya kabila la Manase, kulikuwa na wanaume 18,000 walioitajwa kwa majina ili waje kumweka Daudi kuwa mfalme.

32 Kutoka kwa kabila la Isakari, kulikuwa na viongozi 200 ambao walielewa nyakati na kujua yale ambayo Waisraeli walipaswa kufanya, na ndugu zao wote walikuwa chini ya uongozi wao. **33** Kutoka kwa Zabuloni, kulikuwa na wanaume 50,000 walioweza kutumikia jeshini, waliojipanga kivita wakiwa na silaha zote za vita, wote walijiunga na Daudi kwa ushikamanifu usiogawanyika.* **34** Kutoka kwa Nafthali, kulikuwa na wakuu 1,000, nao walikuwa pamoja na wanaume 37,000 wenye ngao kubwa na mkuki. **35** Kutoka kwa Wadani, wale waliojipanga kivita walikuwa 28,600. **36** Na kutoka kwa Asheri, wale walioweza kutumikia jeshini na kujipanga kivita walikuwa 40,000.

37 Kutoka ng'ambo ya Yordani,^d kutoka kwa Warubeni,

12:28, 30 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 12:33 *Au “wote waliojiunga na Daudi hawakuwa na miyo miwili.”

Wagadi, na nusu ya kabila la Manase, kulikuwa na wanajeshi 120,000 waliokuwa na aina zote za silaha za vita. **38** Hao wote walikuwa wanaume wa vita, walioungana pamoja vitani; walikuja Hebroni kwa moyo kamili ili kumweka Daudi kuwa mfalme wa Israeli yote, na pia Waisraeli wengine wote walikuwa na nia moja ya* kumweka Daudi kuwa mfalme.^a **39** Nao walikaa huko pamoja na Daudi kwa siku tatu, wakila na kunywa, kwa kuwa ndugu zao walikuwa wamefanyia matayarisho kwa ajili yao. **40** Pia majirani wao, na hata wale waliokuwa mbali kufikia Isakari, Zabuloni, na Naftali, walikuwa wakileta vyakula kwa punda, ngamia, nyumbu, na ng'ombe—walileta unga, keki za tini zilizoshinikizwa na keki za zabibu kavu, divai, mafuta, na ng'ombe na kondoo wengi sana, kwa maana watu walishangilia nchini Israeli.

13 Daudi alishauriana na wakuu wa maelfu na wa mamia na kila kiongozi.^b **2** Kisha Daudi akaliaambia kutaniko lote la Waisraeli: “Mkiona ni vema na ikiwa ni jambo linalokubalika kwa Yehova Mungu wetu, acheni tutume ujumbe kwa ndugu zetu waliobaki katika maeneo yote ya Israeli na pia kwa makuhanini na Walawi katika majiji yao^c yenye malisho waje kuungana nasi. **3** Na acheni tulirudishe Sanduku^d la Mungu wetu.” Kwa maana hawakuwa wameilitunza katika siku za Sauli.^e **4** Kutaniko lote likakubali ku-

12:38 *Tnn., “walikuwa na moyo mmoja katika.”

SURA YA 12

a Mwa 49:8, 10
1Nya 11:10

SURA YA 13

b 1Nya 15:25

c Hes 35:2

d 1Sa 7:2

e 1Sa 14:18

Safu ya 2

a Hes 34:2, 8

b 1Sa 6:21-7:1
2Sa 6:1, 2
1Nya 15:3

c Yos 15:9, 12

d Kut 25:22
Hes 7:89
1Sa 4:4
2Sa 6:2

e Kut 37:5

f 2Sa 6:3-8

g Kut 15:20

h 1Nya 25:1

i 2Nya 5:13

j Hes 4:15

k Law 10:1, 2

fanya hivyo, kwa maana watu wote walilionga kuwa jambo jema. **5** Basi Daudi akawakusanya Waisraeli wote, kuanzia mto wa Misri* mpaka Lebo-Hamathi,^{#a} ili walete Sanduku la Mungu wa kweli kutoka Kiriath-yearimu.^b

6 Daudi na Waisraeli wote wakapanda kwenda Baala,^c mpaka Kiriath-yearimu, jiji la Yuda, ili kuleta kutoka huko Sanduku la Mungu wa kweli, Yehova, anayeketi kwenye kiti cha ufalme juu ya* makerubi,^d mahali ambapo watu husali katika jina lake. **7** Hata hivyo, walilitoa Sanduku la Mungu wa kweli katika nyumba ya Abinadabu na kuliweka juu ya gari jipya la kukotwa,^e na Uza na Ahio walikuwa wakiliongoza gari hilo.^f

8 Daudi na Waisraeli wote walikuwa wakisherehekea mbele za Mungu wa kweli kwa nguvu zao zote, kwa nyimbo, vinubi, vinanda vinginevyo, matari,^g matoazi,^h na tarumbe-ta.ⁱ **9** Lakini walipofika kwenye uwanja wa kupuria wa Kidoni, Uza aliunyoosha mkono wake haraka na kulikamata Sanduku hilo, kwa sababu ng'ombe walikuwa karibu kuliangusha. **10** Ndipo hasira ya Yehova ikawaka dhidi ya Uza, Naye akamuua kwa sababu aliunyoosha mkono wake na kulikamata Sanduku^j hilo, naye akafa hapo mbele za Mungu.^k **11** Lakini Daudi akakasirika kwa sababu hasira kali ya Yehova iliwaka dhidi ya Uza; na tangu siku hiyo mahali hapo panaitwa Peres-uza.*

13:5 *Au “kuanzia Shihori huko Misri.”

^{#a}Au “njia ya kuingia Hamathi.” **13:6**

*Au labda, “katikati ya.” **13:11** *Maana yake “Ghadhabu Dhidi ya Uza.”

12 Basi Daudi akamwogopa Mungu wa kweli siku hiyo na kusema: “Ninawezaje kulileta kwangu Sanduku la Mungu wa kweli?”^a 13 Daudi hakulileta Sanduku hilo mahali alipokuwa katika Jiji la Daudi, lakini aliagiza lipelekwe katika nyumba ya Obed-edomu, Mgathi. 14 Sanduku la Mungu wa kweli lilikaa pamoja na watu wa nyumba ya Obed-edomu, likabaki katika nyumba yake kwa miezi mitatu, na Yehova akaendelea kuwabariki watu wa nyumba ya Obed-edomu na vitu vyote alivyokuwa navyo.^b

14 Mfalme Hiram^c wa Tiro aliwatuma waju-mbe kwa Daudi, pamoja na mbao za mierezi, waashi,^{*} na maseremala ili wamjengee Daudi nyumba.^{#d} 2 Na Daudi alijua kwamba Yehova alikuwa amemwimarisha kabisa kuwa mfalme wa Israeli,^e kwa maana ufalme wake ulikuwa ume-kwezwa sana kwa ajili ya watu Wake Waisraeli.^f

3 Daudi alichukua wake^g zaidi huko Yerusalemu, na Daudi akazaa wana na mabinti zaidi.^h 4 Haya ndiyo majina ya watoto wake waliozaliwa Yerusalemu:ⁱ Shamua, Shobab, Nathani,^j Sulemani,^k 5 Ibhari, Elishua, Elpeleti, 6 Noga, Nefegi, Yafia, 7 Elishama, Beeliada, na Eli-feleti.

8 Wafilisti waliposikia kwamba Daudi alikuwa ametiwa mafuta kuwa mfalme wa Waisraeli wote,^l Wafilisti wote wakapanda kuja kumtafuta Daudi.^m Daudi aliposi-

14:1 *Au “wajenzi wa kuta.” #Au “jumba la mfalme.”

SURA YA 13

a 2Sa 6:9-11

b Mwa 30:27
Mwa 39:5

SURA YA 14

c 1Fa 5:6, 8

d 2Sa 5:11, 12

e Zb 89:20, 21

f 2Sa 7:8

g Kum 17:17

h 2Sa 5:13-16

i 1Nya 3:5-9

j Lu 3:23, 31

k 1Fa 1:47
Mt 1:6

l 1Nya 11:3

m 2Sa 5:17
Zb 2:2

Safu ya 2

a 2Sa 5:18, 22
2Sa 23:13

b 2Sa 5:19-21

c Isa 28:21

d Kum 7:25

e 2Sa 5:22-25

f Yos 8:2
Zb 18:34g Kum 23:14
Amu 4:14h Mwa 6:22
Kut 39:32

i Yos 16:10

kia jambo hilo, akaenda kukabiliana nao. 9 Kisha Wafilisti wakaja na kuvamia tena na tena katika Bonde la* Refaimu.^a 10 Daudi akamuuliza Mungu: “Je, nipande kwenenda kuwashambulia Wafilisti? Je, utawatia mikononi mwangu?” Ndipo Yehova akamwambia: “Panda uende, nami hakika nitawatia mikononi mwako.”^b 11 Basi Daudi akapanda kwenenda Baal-perasimu,^c naye akawaua huko. Ndipo Daudi akasema: “Mungu wa kweli amewapasua na kuwapita maadui wangu kwa mkono wangu, kama ufa uliipasuliwa na maji.” Ndiyo sababu walipaita mahali hapo Baal-perasimu.* 12 Wafilisti wakaacha miungu yao hapo, na Daudi alipotoa amri, miungu hiyo iliteketezwa motoni.^d

13 Baadaye Wafilisti waka-ja tena na kuvamia bondeni.^{*e}

14 Daudi akamwomba Mungu ushauri tena, lakini Mungu wa kweli akamwambia: “Usipande moja kwa moja na kuwafuatia. Badala yake, zunguka nyuma yao, uwashambulie mbele ya vichaka vya mibaka.^f

15 Na utakaposikia sauti ya watu wakipiga mwendo juu ya vichaka vya mibaka, washambulie, kwa sababu mimi Mungu wa kweli nitakuwa nime-tangulia mbele yako ili kuliua jeshi la Wafilisti.”^g 16 Basi Daudi akafanya kama Mungu wa kweli alivyomwamuru,^h wakaliua jeshi la Wafilisti kuanzia Gibeoni mpaka Gezeri.ⁱ 17 Umaarufu wa Daudi ukenea katika nchi zote, na Yeho-

14:9 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”

14:11 *Maana yake “Bwana Anayepasua na Kupita.”

14:13 *Au “kwenye nchi tambarare ya chini.”

va akayafanya mataifa yote ya mwogope Daudi.^a

15 Naye akaendelea kujijengea nyumba kati ka Jiji la Daudi, akatayarisha mahali kwa ajili ya Sanduku la Mungu wa kweli na kupiga hema kwa ajili yake.^b

2 Huo ndio wakati ambao Daudi alisema: "Hakuna mtu yeyote anayepaswa kubeba Sanduku la Mungu wa kweli isipokuwa Walawi, kwa maana Yehova amewachagua ili walibebe Sanduku la Yehova na kumhudumia sikuzote."^c

3 Kisha Daudi akawakusanya Waisraeli wote Yerusalemu ili kulipandisha Sanduku la Yehova na kulileta mahali alipotayarisha kwa ajili yake.^d

4 Daudi akawakusanya wazao wa Haruni^e na Walawi;^f

5 kutoka kwa Wakohathi, mkuu Urieli na ndugu zake

120; **6** kutoka kwa Wamerari, mkuu Asaya^g na ndugu zake

220; **7** kutoka kwa Wagershomu, mkuu Yoeli^h

na ndugu zake **130**; **8** kutoka kwa wazao wa Elisafani,ⁱ

mkuu Shemaya na ndugu zake **200**; **9** kutoka kwa wazao wa Hebroni, mkuu Elieli na ndugu zake

80; **10** kutoka kwa wazao wa Uzieli,^j mkuu Aminadabu na ndugu zake **112**.

11 Tena, Daudi akawaita makuhani Sadoki^k na Abiathari^l

na Walawi Urieli, Asaya, Yoeli, Shemaya, Elieli, na Aminadabu,

12 akawaambia: "Ninyi ndio viongozi wa koo* za Walawi. Jitakaseni, ninyi na ndugu zenu, nanyi mlipandishe Sanduku la Yehova, Mungu wa Israeli mpaka mahali ambapo nimetayarisha kwa ajili yake.

15:12 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 14

a Kum 2:25
Kum 11:25
Yos 2:9

SURA YA 15

b 2Sa 7:1, 2
1Nya 16:1
Zb 132:1-5

c Hes 4:15
Kum 10:8

d 2Sa 6:12
1Nya 13:5

e Hes 3:2, 3

f 1Nya 6:1

g 1Nya 6:29, 30

h 1Nya 23:6-8

i Kut 6:18, 22

j Kut 6:16, 18

k 2Sa 8:17

l 1Sa 22:20
1Fa 2:27, 35

Safu ya 2

a 2Sa 6:3

b 2Sa 6:8

c Hes 4:15
Kum 31:9

d Kut 25:14
Hes 4:6
2Nya 5:9

e Zb 33:2

f 1Nya 16:5
2Nya 5:12, 13

g 1Nya 6:31, 33
1Nya 25:5

h 1Nya 6:31, 39
1Nya 25:1, 2
Zb 83:Uta

i 1Nya 6:31, 44

j 1Nya 25:9

k 1Nya 6:31-33

l 1Nya 25:1

m 1Nya 13:8

n Zb 46:Uta

o 1Nya 16:4, 5

p Zb 6:Uta

1 MAMBO YA NYAKATI 15:1-21

13 Kwa kuwa mara ya kwanza hamkulibeba,^a hasira ya Yehova Mungu wetu iliwaka dhidi yetu,^b kwa sababu hatukutafuta utaratibu unaofaa."^c

14 Basi makuhani na Walawi wakajitakasa ili walipandishe Sanduku la Yehova Mungu wa Israeli.

15 Kisha Walawi wakalibeba Sanduku la Mungu wa kweli mabegani mwao kwa kutumia fito zake,^d kama Musa alivyoamuru kwa neno la Yehova. **16** Ndipo Daudi akawaambia wakuu wa Walawi wawaweke ndugu zao waimbaji ili waimbe kwa shangwe na sauti kubwa, kwa ala za muziki: vinanda, vinubi,^e na matoazi.^f

17 Basi Walawi wakamweka Hemani^g mwana wa Yoeli na, kutoka kati ya ndugu zake, Asafu^h mwana wa Berekia na, kutoka kati ya ndugu zao Wamerari, Ethaniⁱ mwana wa Kushaya. **18** Walikuwa pamoja na ndugu zao wa kikundi cha pili,^j Zekaria, Beni, Yaazieli, Shemiramothi, Yehieli, Uni, Eliabu, Benaya, Maaseya, Matithia, Elifelehu, na Mikneya na Obed-edomu na Yeieli wali nzi wa malango. **19** Waimbaji Hemani,^k Asafu,^l na Ethani waliwekwa kupiga matoazi ya shaba;^m **20** na Zekaria, Azieli, Shemiramothi, Yehieli, Uni, Eliabu, Maaseya, na Benaya walipiga vinanda vilivyopatanishwa na sauti ya Alamothi;^{*n} **21** na Matithia,^o Elifelehu, Mikneya, Obed-edomu, Yeieli, na Azazia walipiga vinubi vilivyopatanishwa na sauti ya Shemini-thi,^{*p} ili waongoze uimbaji.

15:20, 21 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

22 Kenania^a mkuu wa Walawi alisimamia usafirishaji, kwa maana alikuwa stadi, **23** na Berekia na Elkana walikuwa walinzii wa malango kwa ajili ya Sanduku. **24** Makuhani Shebania, Yoshafati, Nethaneli, Amasai, Zekaria, Benaya, na Eliezeri walipiga tarumbeta kwa sauti kubwa mbele ya Sanduku la Mungu wa kweli,^b na Obed-edomu na Yehia walitumikia pia wakiwa walinzii wa malango kwa ajili ya Sanduku.

25 Kisha Daudi na wazee wa Israeli na wakuu wa maelfu walikuwa wakitembea kando kando ili kulipandisha sanduku la agano la Yehova kutoka katika nyumba ya Obed-edomu^c wakishangilia.^d **26** Mungu wa kweli alipowasaidia Walawi waliokuwa wakilibeba sanduku la agano la Yehova, waliwatoa dhabihu ng'ombe dume saba wachanga na kondoo dume saba.^e **27** Daudi alikuwa amevaa joho lisilo na mikono la kitambaa bora, kama walivyovaa Walawi wote waliobeba Sanduku hilo, waimbaji, na Kenania mkuu wa usafirishaji na wa waimbaji; Daudi pia alikuwa amevaa efodi ya kitani.^f **28** Waisraeli wote walikuwa wakilipandisha sanduku la agano la Yehova kwa kelele za shangwe,^g wakipiga pembe, tarumbeta,^h matoazi, na kupiga kwa sauti kubwa vinanda na vinubi.ⁱ

29 Lakini sanduku la agano la Yehova lilipofika kwenye Jiji la Daudi,^j Mikali, binti ya Sauli,^k akaangalia chini kupitia dirishani, akamwona Mfalme Daudi akirukaruka na kusherehekea; akaanza kumdharau moyoni mwake.^l

SURA YA 15

a 1Nya 15:27

b 1Nya 16:4, 6

c 1Nya 13:14

d 2Sa 6:4, 5
2Sa 6:12

e 2Sa 6:13

f 2Sa 6:14, 15

g 1Nya 13:8

h 1Nya 16:4, 6

i 2Sa 6:5

j 1Nya 17:1

k 1Sa 18:27
2Sa 3:13, 14

l 2Sa 6:16

Safu ya 2

SURA YA 16

a 1Fa 8:1
1Nya 15:1b 2Sa 6:17-19
1Fa 8:5

c Law 1:3

d Law 3:1

e Hes 18:2

f 1Nya 6:31, 39

g 1Nya 15:18

h 1Nya 15:21

i 1Nya 15:17, 19

j 1Nya 6:31, 39

k Zb 106:1

l Zb 67:2
Zb 105:1-6
Isa 12:4m 2Sa 23:1
Efe 5:19

16 Basi wakaliingiza Sanduku la Mungu wa kweli na kuliweka ndani ya hema ambalo Daudi alikuwa amepiga ili aliweke humo;^a nao wakatoa dhabihu za kuteketeza na dhabihu za ushirika mbele za Mungu wa kweli.^b **2** Daudi alipomaliza kutoa dhabihu za kuteketezwa^c na dhabihu za ushirika,^d akawabariki watu katika jina la Yehova. **3** Isitoshe, aliwagawia Waisraeli wote, kila mwanamume na mwanamke, mka-te mmoja wa mviringo, keki ya tende, na keki ya zabibu kavu. **4** Kisha akawaweka baadhi ya Walawi wahudumu mbele ya Sanduku la Yehova,^e wamheshimu,* wamshukuru, na kumsifu Yehova Mungu wa Israeli. **5** Asafu^f alikuwa kiongozi, na wa pili Zekaria; naye Yeieli, Shemiramothi, Yehieli, Matithia, Eliabu, Benaya, Obed-edomu, na Yeieli^g walipiga vinanda na vinubi;^h na Asafu alipiga matoazi,ⁱ **6** na makuhani Benaya na Yahaziel walipiga tarumbeta daima mbele ya sanduku la agano la Mungu wa kweli.

7 Hiyo ndiyo siku ambayo Daudi kwa mara ya kwanza alitunga* wimbo huu wa kumshukuru Yehova na kumwagiza Asafu^j na ndugu zake wauimbe:

8 "Mshukuruni Yehova,^k liitieni jina lake,
Yajulisheni mataifa mate-
ndo yake!^l

9 Mwimbieni, mwimbieni
sifa,*^m

16:4 *Tnn., "wamkumbuke." **16:7** *Au "alichangia." **16:9** *Au "mpigieni muziki."

- Tafakarini* kazi zake zote zinazostaajabisha.^a
- 10** Jivunieni jina lake takatifu.^b
- Mioyo ya wale wanamotoafuta Yehova na ishangilie.^c
- 11** Mtafuteni Yehova^d na nguvu zake, Utafuteni uso* wake daima.^e
- 12** Kumbukeni kazi zinazostaajabisha alizofanya,^f Miujiza yake na hukumu alizotangaza,
- 13** Enyi uzao wa* Israeli mtumishi wake,^g Enyi wana wa Yakobo, watu wake aliowachagua.^h
- 14** Yeye ni Yehova Mungu wetu.ⁱ Hukumu zake ziko duniani kote.^j
- 15** Kumbukeni agano lake milele, Ahadi aliyotoa,* hata kufikia vizazi elfu,^k
- 16** Agano alilofanya na Abrahamu,^l Na kiapo alichomwapia Isaka,^m
- 17** Alichotoa kama amri kwa Yakoboⁿ Na kama agano la kudumu kwa Israeli,
- 18** Akisema, 'Nitakupa nchi ya Kanaani^o Kuwa urithi wako ulioga-wiwa.^p
- 19** Mlipokuwa wachache, Naam, wachache sana, nanyi mlikuwa wageni nchini.^q

16:9 *Au labda, "Zungumzeni kuhusu."
16:11 *Au "uwepo." **16:13** *Au "wazao wa." Tnn., "mbegu ya." **16:15** *Tnn., "Neno aliloamuru."

SURA YA 16

a Zb 107:43

b Law 22:32
Isa 45:25
Yer 9:24c 1Nya 28:9
Flp 4:4d Amo 5:4
Sef 2:3

e Zb 24:5, 6

f Zb 111:2-4

g Isa 41:8

h Zb 135:4

i Zb 95:7

j Zb 105:7-11

k Kum 7:9

l Mwa 15:18
Mwa 17:1, 2

m Mwa 26:3-5

n Mwa 28:14

o Mwa 12:7
Mwa 17:8
Mwa 35:12

p Kum 32:8

q Mwa 34:30
Kum 26:5
Zb 105:12-15

Safu ya 2

a Mwa 20:1
Mwa 46:6

b Mwa 31:7, 42

c Mwa 12:17
Mwa 20:3

d Mwa 20:7

e Zb 40:10
Zb 96:1-6

f Kut 15:11

g Isa 45:20
1Ko 8:4

h Isa 44:24

i Kum 33:26
Zb 8:1

j 1Ti 1:11

k Zb 68:34
Zb 96:7-13l Kum 28:58
Ne 9:5
Zb 148:13

1 MAMBO YA NYAKATI 16:10-29

- 20** Walitembeatembea kuto-ka taifa moja hadi taifa lingine, Kutoka ufalme mmoja hadi ufalme mwingine.^a
- 21** Hakumruhusu mtu yeyote awakandamize,^b Lakini kwa sababu yao aliwakaripia wafalme,^c
- 22** Akisema, 'Msiwaguse watiwa-mafuta wangu, Wala msiwatendee manabii wangu jambo lolote baya.'^d
- 23** Mwimbieni Yehova, dunia yote! Tangazeni wokovu wake siku baada ya siku!^e
- 24** Tangazeni utukufu wake miongoni mwa mataifa, Kazi zake zinazostaajabisha miongoni mwa mataifa yote.
- 25** Kwa maana Yehova ni mkuu na anastahili kusi-fiwa kuliko wote. Anaogopesha kuliko miungu mingine yote.^f
- 26** Miungu yote ya mataifa ni miungu ya ubatili,^g Lakini Yehova ndiye aliyeziumba mbingu.^h
- 27** Mbele zake kuna utukufu* na fahari;ⁱ Katika makao yake kuna nguvu na shangwe.^j
- 28** Mpeni Yehova anachostahili, enyi familia za mataifa, Mpeni Yehova anachostahili kwa sababu ya utukufu wake na nguvu zake.^k
- 29** Mpeni Yehova utukufu ambao jina lake linastahili;^l

16:27 *Au "adhama."

Leteni zawadi na mje mbele zake.^a

Mwinamieni* Yehova katika mapambo matakatifu.^{#b}

30 Tetemekeni mbele zake, dunia yote!

Dunia imeimarishwa kabisa; haiwezi kusogezwa.*^c

31 Mbingu na zishangilie, dunia na iwe na shangwe;^d Tangazeni miongoni mwa mataifa: 'Yehova amekuwafalme!'^e

32 Bahari na ingurume na vitu vyote vinavyojaza; Mashamba na vitu vyote vilivyomo na vishangilie.

33 Wakati uleule miti ya msituni na ishangilie kwa sauti mbele za Yehova, Kwa maana anakuja* kuhukumu dunia.

34 Mshukuruni Yehova, kwa maana yeye ni mwema;^f Upendo wake mshikamanifu unadumu milele.^g

35 Nanyi semeni, "Tuokoe, Ee Mungu wa wokovu wetu,^h Tukusanye na kutuokoa kutoka katika mataifa, Ili tulishukuru jina lako takatifu! Na tushangilie kukusifu wewe.ⁱ

36 Yehova, Mungu wa Israeli, na asifiwe Kwa umilele wote."[#]

Na watu wote wakasema, "Amina!"[#] nao wakamsifu Yehova.

16:29 *Au "Mwabuduni." #Au labda, "kwa sababu ya fahari ya utakatifu wake." 16:30 *Au "kutikiswa; kufanywa ipepesuke." 16:33 *Au "amekuja." 16:36 *Au "milele na milele." #Au "Na iwe hivyo!"

SURA YA 16

a 1Nya 29:3-5
Mt 5:23

b Kum 26:10

c Zb 104:5
Mhu 1:4

d Zb 97:1

e Ufu 19:6

f 2Nya 5:13
Lu 18:19

g Zb 103:17
Yer 31:3
Omb 3:22

h Zb 68:20

i Zb 122:4

j Isa 43:21

Safu ya 2

a 1Nya 15:16, 17

b 1Nya 16:4-6

c Kut 29:38
2Nya 13:11
Ezr 3:4

d 1Nya 12:28

e 1Fa 3:4

f Kut 29:39
2Nya 2:4

g 1Nya 25:1

h 1Nya 16:4

i 2Nya 5:13
Ezr 3:11

j 1Nya 6:31, 33
1Nya 15:16, 17

k 1Nya 25:1, 3

SURA YA 17

l 1Fa 1:8
1Nya 29:29

m 1Nya 14:1

37 Kisha Daudi akamwacha Asafu^a na ndugu zake hapo mbele ya sanduku la agano la Yehova ili wahudumu daima mbele ya Sanduku^b hilo, kulingana na utaratibu wa kila siku.^c **38** Obed-edomu na ndugu zake, watu 68, na Obed-edomu mwana wa Yeduthuni, na Hosa walikuwa walenzi wa malango; **39** na kuhani Sadoki^d na makuhani wenzake walikuwa mbele ya hema la ibada la Yehova mahali pa juu kule Gibeoni^e **40** ili wamtolee Yehova kwa ukawaida dhambi za kuteketezwa kwenye madhabahu ya dhambi za kuteketezwa, asubuhi na jioni, na kufanya mambo yote ya-liyoandikwa katika Sheria ya Yehova aliyowaamuru Waisraeli wafuate.^f **41** Walikuwa pamoja na Hemani na Yeduthuni^g na wanaume wengine waliochaguliwa na kutajwa majina ili wamshukuru Yehova,^h kwa sababu "upeendo wake mshikamanifu unadumu milele";ⁱ **42** nao walikuwa pamoja na Hemani/ na Yeduthuni ili wapige tarumbeta, matoazi, na ala zilizotumiwa kumsifu* Mungu wa kweli; na wana wa Yeduthuni^k walikuwa langoni. **43** Kisha watu wote wakaenda nyumbani kwao, na Daudi akaenda kuwabariki watu wa nyumba yake mwenyewe.

17 Mara tu Daudi alipoanzza kuishi katika nyumba yake mwenyewe,* alimwambia hivi nabii Nathani:^l "Mimi hapa ninaishi katika nyumba ya mierezi^m huku sanduku la agano la Yehova liki-

16:42 *Au "na ala za wimbo wa." 17:1 *Au "jumba lake mwenyewe la mfalme."

wa ndani ya vitambaa vya mahema.”^a **2** Nathani akamwambia Daudi: “Fanya jambo lote lililo moyoni mwako, kwa sababu Mungu wa kweli yuko pamoja nawe.”

3 Usiku huohuo, neno hili la Mungu likamjia Nathani: **4** “Nenda ukamwambie mtumishi wangu Daudi, ‘Yehova anasema hivi: “Si wewe utakayenijengea nyumba nitakayokaa ndani yake.”^b **5** Kwa maana sijakaa ndani ya nyumba tangu siku nilipowatoa nje Waisraeli mpaka leo, bali nimekuwa nikihama hema moja hadi hema lingine na kutoka hema moja la ibada hadi hema lingine la ibada.”^c **6** Wakati wote nilipotembea na Waisraeli wote, je, niliwahi wakati wote kumuuliza mwamuzi yeyote wa Israeli niliyemweka awachunge watu wangu, ‘Kwa nini hukunijengea nyumba ya mierezi?’”

7 “Sasa mwambie hivi mtumishi wangu Daudi: ‘Yehova wa majeshi anasema hivi: “Nilikutoa malishoni, ili usiendelee kuchunga kondoo, uwe kiongozi wa watu wangu Waisraeli.”^d **8** Nami nitakuwa pamoja nawe popote utakapoenda,^e nami nitawaangamiza maadui wako wote kutoka mbele yako;^f nami nitakujeungea jina kama jina la watu maarufu duniani.”^g **9** Nita-chagua mahali kwa ajili ya watu wangu Waisraeli na kuwaweka humo, nao wataishi humo na hawatasumbuliwa tena; na watu waovu hawatawakandamiza* tena kama wa-

17:5 *Labda inamaanisha “kutoka kambini moja ya mahema hadi nyingine na kutoka eneo moja la kuishi hadi lingine.”
17:9 *Tnn., “hawatawachosha.”

SURA YA 17

a 2Sa 7:1-3
1Nya 15:1
2Nya 1:4

b 2Sa 7:4-7
1Fa 8:17-19
1Nya 22:7, 8

c Kut 40:2
Hes 4:24, 25
2Sa 6:17
Zb 78:60

d 1Sa 16:11, 12
1Sa 17:15
1Sa 25:30
2Sa 7:8-11
Zb 78:70, 71

e 1Sa 18:14
2Sa 8:6

f 1Sa 25:29
1Sa 26:10
Zb 89:20, 22

g 1Sa 18:30

Safu ya 2

a Kut 2:23

b Amu 2:16

c Zb 18:40

d 1Fa 8:20
Zb 132:11

e 2Sa 7:12-17
1Fa 9:5
1Nya 28:5
Yer 23:5

f 1Fa 5:5
1Nya 22:10

g Zb 89:3, 4
Isa 9:7
Da 2:44

h 2Sa 7:14
Lu 9:35
Ebr 1:5

i Isa 55:3

j 1Sa 15:24, 28
1Nya 10:13, 14

k Da 2:44
Yoh 1:49
2Pe 1:11

l Zb 89:36
Yer 33:20, 21
Lu 1:32, 33
Ebr 1:8
Ufu 3:21

m 2Sa 7:8
2Sa 7:18-20

n Mt 22:42
Mdo 13:34
Ufu 22:16

livyofanya zamani,^a **10** tangu siku nilipowaweka waa-muzi juu ya watu wangu Waisraeli.^b Nami nitawashinda maadui wako wote.^c Pia, ninakuambia, ‘Yehova atakujeungea nyumba.’^{*}

11 ““Siku zako zitakapokwisha nawe uzikwe pamoja na mababu zako, nitamwinua mzao wako* baada yako, mmoja wa wana wako,^d nami nitauimarisha kabisa ufalme wake.^e **12** Yeye ndiye atakayenijengea nyumba,^f nami nitakii-marisha kabisa kiti chake cha ufalme milele.^g **13** Nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwangu.^h Sitauondoa upendo wangu mshikamanifu kutoka kwakeⁱ kama nilivyoundoa kutoka kwa yule aliyekutangulia.^j **14** Nitamfanya asimame katika nyumba yangu na katika ufalme wangu milele,^k na kiti chake cha ufalme kitadumu milele.””^l

15 Nathani alimwambia Daudi maneno hayo yote na maono hayo yote.

16 Ndipo Mfalme Daudi akaingia na kuketi mbele za Yehova na kusema: “Mimi ni nani, Ee Yehova Mungu? Na nyumba yangu ni nini hivi kwamba umenileta mpaka hapa nilipofika?^m **17** Na kana kwamba hilo halitoshi, Ee Mungu, unasema pia kwamba nyumba yangu mimi mtumishi wako itadumu kwa muda mrefu,ⁿ nawe umeniona kuwa mtu anayepaswa kukwezwa zaidi,^{*} Ee Yehova Mungu. **18** Mimi mtumishi wako Daudi nitakwambia nini zaidi kuhusu heshima uliyonipa

17:10 *Au “ukoo wa kifalme.” 17:11 *Tnn., “nitainua mbegu yako.” 17:17 *Au “mtu mwenye cheo kikubwa.”

na wewe unanijua vizuri sana mimi mtumishi wako?^a

19 Ee Yehova, kwa ajili yangu mimi mtumishi wako na kupatana na moyo wako* ume-tenda mambo haya yote makuu kwa kufunua ukuu wako.^b

20 Ee Yehova, hakuna aliye kama wewe,^c na hakuna Mungu ila wewe;^d mambo yote tuliyoosikia kwa masikio yetu yanathibitisha jambo hilo.

21 Na kuna taifa gani lingine duniani lililo kama watu wako Waisraeli?^e Wewe Mungu wa kweli ulienda na kuwakomboa wakiwa watu wako.^f Ulijijengea jina kwa matendo yako makuu na yenye kuogopesha,^g ukayafukuza mataifa kutoka mbele ya watu wako^h uliowakomboa kutoka Misri.

22 Uliwafanya watu wako Waisraeli wawe watu wako milele;ⁱ na wewe, Ee Yehova, ukawa Mungu wao.^j

23 Sasa, Ee Yehova, ahadi uliyotoa kunihusu mimi mtumishi wako na nyumba yangu na ithibitike kuwa ya uaminifu milele, na ufanye kama ulivyoahidi.^k

24 Jina lako na lidumu na kukwezwa^l milele, ili watu waseme, 'Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, ni Mungu kwa Israeli,' na nyumba yangu mimi mtumishi wako Daudi na iimarishwe kabisa mbele zako.^m

25 Kwa maana wewe, Mungu wangu, umenifunulia mimi mtumishi wako kusudi lako la kunijengea nyumba.* Ndiyo sababu mimi mtumishi wako nina ujasiri wa kutoa sala hii kwako.

26 Na sasa, Ee Yehova, wewe ndiye Mungu wa kweli, nawe umeahidi mambo haya mema ku-

17:19 * Au "kulingana na mapenzi yako."
17:25 * Au "ukoo wa kifalme."

SURA YA 17

a Zb 139:1

b 2Sa 7:21-24

c Kut 15:11

d Isa 43:10

e Kum 4:7
Zb 147:20f Kut 19:5
Zb 77:15g Kum 4:34
Ne 9:10
Isa 63:12
Eze 20:9h Kum 7:1
Yos 10:42
Yos 21:44

i 1Sa 12:22

j Mwa 17:7
Kum 7:6, 9

k 2Sa 7:25-29

l 2Nya 6:33
Zb 72:19
Mt 6:9
Yoh 12:28

m Zb 89:35, 36

Safu ya 2

SURA YA 18

a 1Sa 5:8
2Sa 1:20

b 2Sa 8:1

c Hes 24:17
Zb 60:8d 2Sa 8:2
2Fa 3:4

e 1Fa 11:23

f 1Sa 14:47
2Sa 10:6
Zb 60:Uta

g 2Nya 8:3

h Mwa 15:18
Kut 23:31
2Sa 8:3, 4

i Zb 20:7

j Kum 17:16
Zb 33:17

k 2Sa 8:5-8

l 1Nya 17:8

nihusu mimi mtumishi wako. **27** Basi na ufurahie kuibariki nyumba yangu mimi mtumishi wako, na idumu milele mbele zako, kwa sababu wewe, Ee Yehova, umeibariki, nayo imebarikiwa milele."

18 Wakati fulani baadaye, Daudi aliwashinda Wafilisti na kuwatiisha, akachukua jiji la Gathi^a na miji yake kutoka mikononi mwa Wafilisti.^b

2 Kisha akawashinda Wamoabu,^c na Wamoabu wakawa watumishi wa Daudi na kumletea ushuru.^d

3 Daudi alimshinda Mfalme Hadadezeri^e wa Soba^f karibu na Hamathi^g alipokuwa akienda kuimarisha mamlaka yake katika eneo la Mto Efrati.^h

4 Daudi akateka magari 1,000 ya vita, wapanda farasi 7,000, na wanajeshi 20,000 wanaotembea kwa miguu.ⁱ

Kisha Daudi akawakata farasi wote mishipa ya miguu isipokuwa farasi 100 waliokokota magari.^j

5 Wasiria wa Damasko walipokuja kumsaidia Mfalme Hadadezeri wa Soba, Daudi aliwaua Wasiria 22,000.^k

6 Halafu Daudi akaweka kambi za kijeshi kule Siria ya Damasko, na Wasiria wakawa watumishi wa Daudi na kumletea ushuru. Yehova alimpa Daudi ushindi* popote alipoenda.^l

7 Isitoshe, Daudi alichukua ngao za mviringo za dhahabu kutoka kwa watumishi wa Hadadezeri na kuzileta Yerusalemu.

8 Daudi alichukua shaba nyingi sana kutoka Tibhathi na Kuni, majiji ya Hadadezeri. Sulemani alitumia kutengenezea Bahari

18:6 * Au "wokovu."

ya Shaba,^a nguzo, na vyombo vya shaba.^b

9 Mfalme Tou wa Hamathi aliposikia kwamba Daudi alikuwa amelishinda jeshi lote la Mfalme Hadadezeri^c wa Soba,^d **10** mara moja alimtumama Hadoramu mwana wake kwa Mfalme Daudi ili amjulie hali na kumpongeza kwa sababu alikuwa amepigana na Hadadezeri na kumshinda (kwa maana mara nyingi Hadadezeri alimshambulia Tou), na Hadoramu alimletea Daudi kila aina ya vitu vya dhahabu, fedha, na shaba. **11** Mfalme Daudi akavitakasa vitu hivyo ili viwe vya Yehova,^e pamoja na fedha na dhahabu aliyokuwa amechukua kutoka kwa mataifa yote: kutoka kwa Waedomu na Wamoabu, kutoka kwa Waamoni,^f Wafilisti,^g na Waamaleki.^h

12 Abishaiⁱ mwana wa Seruya^j aliwaua Waedomu 18,000 katika Bonde la Chumvi.^k

13 Aliweka kambi za kijeshi huko Edomu, na Waedomu wote wakawa watumishi wa Daudi.^l Yehova alimpa Daudi ushindi* popote alipoenda.^m

14 Daudi akaendelea kutawala Israeli yote,ⁿ naye aliwatawala watu wake wote kwa haki na uadilifu.^o **15** Yoabu mwana wa Seruya alikuwa mkuu wa jeshi,^p Yehoshafati^q mwana wa Ahiludi alifanya kazi ya kuweka kumbukumbu, **16** Sadoki mwana wa Ahitubu na Ahimeleki mwana wa Abiathari walikuwa makuhani, na Shavsha alikuwa mwandishi. **17** Benaya mwana wa Yehoyada aliwasimamia Wakerehti^r na Wapelethi.^s Na wana wa

18:13 *Au "wokovu."

SURA YA 18

a 1Fa 7:23

b 1Fa 7:15, 45

c 2Sa 8:3

d 2Sa 8:9-11

e Yos 6:19
2Nya 5:1

f 1Nya 20:1

g 2Sa 5:25

h 1Sa 27:8, 9
1Sa 30:18, 20

i 1Sa 26:6
2Sa 3:30
2Sa 10:10
2Sa 20:6
2Sa 21:17

j 1Nya 2:15, 16

k 2Sa 8:13, 14

l Mwa 25:23
Mwa 27:40

m Zb 18:48
Zb 144:10

n 1Fa 2:11

o 2Sa 8:15-18
2Sa 23:3, 4
Zb 78:70-72

p 1Nya 11:6

q 1Fa 4:3

r 1Sa 30:14
Sef 2:5

s 1Fa 1:38

Safu ya 2

SURA YA 19

a 2Sa 10:1-5

b 2Sa 9:7

c Mwa 19:36, 38

d Law 19:27

e 1Fa 16:34

Daudi walikuwa na cheo cha kwanza baada ya mfalme.

19 Baadaye Nahashi mfalme wa Waamoni akafa, na mwanawe akawa mfalme baada yake.^a **2** Ndipo Daudi akasema: "Nitamtendea kwa upendo mshikamanifu^b Hanuni mwana wa Nahashi, kwa sababu baba yake alinite ndea kwa upendo mshikamanifu." Basi Daudi akawatuma wajumbe ili wamfariji baada ya kufiwa na baba yake. Lakini watumishi wa Daudi walipofika katika nchi ya Waamoni^c kumfariji Hanuni, **3** wakuu wa Waamoni wakamwambia Hanuni: "Je, unafikiri kwamba Daudi anawatuma wafariji kwako ili kumheshimu baba yako? Je, watumishi wake hawajaja kwako ili kufanya uchunguzi kamili na kukupindua wewe na kuipeleleza nchi?" **4** Kwa hiyo Hanuni akawachukua watumishi wa Daudi, akawanyoa,^d akakata nguo zao katikati kwenye matako na kuwafukuza. **5** Daudi alipoambiwa kuhusu wanaume hao, mara moja akawatuma wanaume wengine waende kukutana nao, kwa sababu wanaume hao walikuwa wameaibishwa sana; mfalme akawaambia: "Kaeni Yeriko^e mpaka ndevu zenu zitakapoota, kisha mrudi."

6 Baada ya muda Waamoni wakaona kuwa wanauka mbele ya Daudi, kwa hiyo Hanuni na Waamoni wakatumama talanta 1,000 za fedha* ili kukodi magari ya vita na wapanda farasi kutoka Mesopotamia,^f Aram-maaka, na

19:6 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. ^fTnn., "Aram-naharaimu."

Soba.^a 7 Basi wakakodi magari 32,000 ya vita, pamoja na mfalme wa Maaka na watu wake. Kisha wakaja na kupiga kambi mbele ya Medeba.^b Waamoni wakakusanyika pamoja kutoka katika majiji yao, wakaja ili kupigana vita.

8 Daudi aliposikia habari hizo, alimtuma Yoabu^c na jeshi lote, kutia ndani mashujaa wake hodari zaidi.^d 9 Nao Waamoni wakatoka na kujipanga kivita kwenye lango la jiji huku wafalme waliokuja wakiwa peke yao uwanjani.

10 Yoabu alipoona kwamba anashambuliwa upande wa mbele na wa nyuma, alichagua baadhi ya wanajeshi bora Israeli na kuwapanga kivita ili wapigane na Wasiria.^e

11 Wanaume waliobaki aliwaweka chini ya usimamizi wa* Abishai ndugu yake,^f ili awapange kivita kupigana na Waamoni. 12 Kisha akasema: "Ikiwa Wasiria^g watanizidi nguvu, basi mtaniokoa; lakini Waamoni wakiwazidi ninyi nguvu, nitawaokoa. 13 Ni lazima tuwe imara na jasiri^h kwa ajili ya watu wetu na kwa ajili ya majiji ya Mungu wetu, naye Yehova atafanya yaliyo mema machoni pake."

14 Kisha Yoabu na wanaume wake wakasonga mbele kwenda kupigana vita na Wasiria, nao wakamkimbia.ⁱ 15 Waamoni walipoona kwamba Wasiria wamekimbia, wakamkimbia pia Abishai ndugu yake na kuingia jijini. Baada ya hayo, Yoabu akarudi Yerusalemu.

16 Wasiria walipoona kwamba wameshindwa na Wais-

19:11 * Tnn., "mikononi mwa."

SURA YA 19

a 1Sa 14:47
2Sa 8:3
2Sa 10:6

b Yos 13:8, 9

c 2Sa 8:16

d 2Sa 10:7, 8
2Sa 23:8

e 2Sa 10:9-12

f 1Nya 11:20, 21

g 2Sa 8:5

h Kum 31:6
Yos 1:9

i Law 26:7, 8
Kum 28:7
2Sa 10:13, 14

Safu ya 2

a 2Sa 8:3

b 2Sa 10:15, 16

c 2Sa 10:17-19

d Zb 18:39

e 1Nya 14:17
Zb 18:44

SURA YA 20

f 1Nya 11:6

g Kum 3:11

h 2Sa 11:1

i 2Sa 12:26

j 2Sa 8:11, 12
2Sa 12:30, 31

raeli, waliwatuma wajumbe wawaite Wasiria waliokuwa katika eneo la Mto Efrati,^a wakiongozwa na Shofaki mkuu wa jeshi la Hadadezeri.^b

17 Daudi alipoambiwa habari hiyo, akawakusanya Waisraeli wote mara moja, wakavuka Yordani na kuwafikia, wakajipanga kivita ili kupigana nao. Daudi alijipanga kivita ili kupigana na Wasiria, nao wakapigana naye.^c 18 Lakini Wasiria waliwakimbia Waisraeli; Daudi akawaua Wasiria 7,000 walioendesha magari ya vita na wanajeshi 40,000 waliotembea kwa miguu, akamua Shofaki mkuu wa jeshi.

19 Watumishi wa Hadadezeri walipoona kwamba wameshindwa na Waisraeli,^d mara moja wakafanya amani na Daudi, wakawa watumishi wake;^e na Wasiria hawakutaka kuwasaidia tena Waamoni.

20 Mwanzoni mwa mwaka,* wakati ambapo wafalme huenda vitani, Yoabu^f aliwaongoza wanajeshi vitani, wakaiharibu nchi ya Waamoni; Yoabu akaenda na kuzingira Raba,^g lakini Daudi akabaki Yerusalemu.^h Yoabu alishambulia jiji la Raba na kulibomoa kabisa.ⁱ 2 Kisha Daudi akachukua taji lililokuwa kwenye kichwa cha Malkamu, akapata kwamba uzito wa taji hilo ulikuwa talanta moja* ya dhahabu, nalo lilikuwa na mawe yenye thamani; Daudi akavishwa taji hilo kichwani. Alichukua pia nyara nyingi sana kutoka katika jiji hilo.^j 3 Akawatoa nje

20:1 * Yaani, majira ya kuchipua. 20:2 * Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

watu waliokuwa ndani yake, akawapa kazi^a ya kukata mawe kwa misumeno na kufanya kazi kwa vifaa vya chuma vyenye ncha kali na kwa mashoka. Hivyo ndivyo Daudi alivyofanya katika majiji yote ya Waamoni. Hatimaye Daudi na wanajeshi wote wakarudi Yerusalemu.

4 Baada ya hayo, wakapigana tena na Wafilisti kule Gezeri. Wakati huo Sibekai^b Mhusha alimuua Sipai, aliyekuwa mzao wa Warefaimu,^c nao wakatiishwa.

5 Wakapigana tena na Wafilisti, na Elhanani mwana wa Yairi akamuua Lahmi ndugu ya Goliathi^d Mgathi, aliyekuwa na mkuki wenye mpini kama mti wa wafumaji wa nguo.^e

6 Vita vikatokea tena huko Gathi,^f ambako kulikuwa na mwanamume mkubwa isivyo kawaida,^g mwenye vidole 6 katika kila mkono na vidole 6 katika kila mguu, jumla ya vidole 24; naye pia alikuwa mzao wa Warefaimu.^h **7** Aliendelea kuwadhihakiⁱ Waisraeli. Basi Yonathani mwana wa Shimea,^j ndugu ya Daudi, akamuua.

8 Watu hao walikuwa wazao wa Warefaimu^k huko Gathi,^l na Daudi na watumishi wake ndio waliowaua.

21 Kisha Shetani* akasimama dhidi ya Waisraeli na kumchochea Daudi awahesabu Waisraeli.^m **2** Basi Daudi akamwambia Yoabuⁿ na wakuu wa watu: “Nendeni mka-wahasabu Waisraeli kuanzia Beer-sheba mpaka Dani;^o kisha mniletee habari ili nijue idadi yao.” **3** Lakini Yoabu akasema: “Yehova na azidishe

SURA YA 20

a 1Fa 9:20, 21

b 2Sa 21:18
1Nya 11:26, 29

c Kum 3:13

d 1Sa 17:4, 7
1Sa 21:19e 2Sa 21:19
1Nya 11:23, 24f Yos 11:22
1Sa 7:14g Hes 13:33
Kum 2:10
Kum 3:11h 2Sa 21:16
2Sa 21:20-22i 1Sa 17:10
2Fa 19:22

j 1Nya 2:13

k Kum 2:11

l 1Sa 17:4

SURA YA 21

m 2Sa 24:1-3

n 2Sa 8:16

o Amu 18:29
2Sa 17:11

Safu ya 2

a 2Sa 24:4, 8

b 2Sa 24:9

c Hes 1:47

d 1Nya 27:23, 24

e 2Sa 12:13

f Zb 25:11
Zb 51:1

g 2Sa 24:10-14

h 1Nya 29:29

i Law 26:26

j Law 26:14, 17

idadi ya watu wake mara 100! Bwana wangu mfalme, hao wote tayari ni watumishi wako bwana wangu, sivyo? Kwa nini bwana wangu unataka kufanya hivyo? Kwa nini uwafanye Waisraeli wawe na hatia?”

4 Lakini neno la mfalme likawa na nguvu kuliko neno la Yoabu. Basi Yoabu akaondoka na kusafiri kotekote Israeli, kisha akarudi Yerusalemu.^a **5** Basi Yoabu akampa Daudi idadi ya watu walioandikishwa. Wanaume wote wa Israeli waliojihami kwa mapanga walikuwa 1,100,000, na wanaume wa Yuda waliojihami kwa mapanga walikuwa 470,000.^b **6** Lakini hakuwaandikisha watu wa kabila la Lawi na Benjamini miongoni mwao,^c kwa sababu neno la mfalme lilimchukiza Yoabu.^d

7 Basi jambo hilo halikumpendeza hata kidogo Mungu wa kweli, kwa hiyo akawalletea Waisraeli ugonjwa hatari. **8** Basi Daudi akamwambia Mungu wa kweli: “Nimetenda dhambi^e kubwa kwa kufanya jambo hili. Na sasa, tafadhali, nisamehe kosa langu mimi mtumishi wako,^f kwa maana nimetenda kwa upumbavu sana.”^g **9** Kisha Yehova akamwambia hivi Gadi,^h mwonaji wa Daudi: **10** “Nenda ukamwambie Daudi, ‘Yehova anasema hivi: “Ninakupa mambo matatu ya kuchagua. Chagua jambo nitakalokutenda.””

11 Basi Gadi akaenda kwa Daudi na kumwambia, “Yehova anasema hivi: ‘Chagua **12** ikiwa unataka miaka mitatu ya njaa kali,ⁱ au ikiwa unataka maadui wako wakufagilie mbali kwa miezi mitatu huku upanga wao ukikuandama,^j au

siku tatu za upanga kutoka kwa Yehova—nchi ikumbwe na ugonjwa hatari^a—huku malai-ka wa Yehova akileta maangamizi^b katika eneo lote la Israeli.^c Sasa fikiria jibu ninalopaswa kumpa Yule aliyenituma.”
13 Kwa hiyo Daudi akamwambia Gadi: “Jambo hilo lina-nihuzunisha sana. Tafadhali, acha nianguke mkononi mwa Yehova, kwa maana rehema zake ni nyingi sana;^c lakini usiniache nianguke mkononi mwa mwanadamu.”^d

14 Ndipo Yehova akaleta ugonjwa hatari^e Israeli hivi kwamba watu 70,000 miongoni mwa Waisraeli wakafa.^f
15 Zaidi ya hilo, Mungu wa kweli alimtuma malaika kati-tika jiji la Yerusalemu ili ku-liangamiza; lakini alipokuwa karibu kuliangamiza, Yehova akaona jambo hilo na kughai-ri* kwa sababu ya msiba huo,^g akamwambia malaika aliye-kuwa akiwaangamiza watu: “Imetoshali^h Sasa shusha mko-no wako.” Malaika wa Yehova alikuwa amesimama karibu na uwanja wa kupuria nafaka wa Ornaniⁱ Myebusi.^j

16 Daudi alipoinua macho yake, alimwona malaika wa Yehova akiwa amesimama kati ya dunia na mbingu aki-wa ameshika mkononi mwa-ke upanga uliochomolewa^k na kuelekezwa Yerusalemu. Mara moja, Daudi na wazee, waki-wa wamevaa nguo za magu-nia,^l wakajiangusha chini kifudufudi.^m
17 Daudi akamwambia Mungu wa kweli: “Je, si mimi niliyesema watu wahesa-biwe? Mimi ndiye niliyetenda dhambi, na mimi ndiye nili-

SURA YA 21

a Law 26:25

b 2Fa 19:35

c Kut 34:6
Zb 51:1
Isa 55:7
Omb 3:22

d 2Nya 28:9

e Hes 16:46

f 2Sa 24:15, 16

g Kut 32:14
Kum 32:36

h Zb 90:13

i 2Nya 3:1

j 2Sa 5:6

k Hes 22:31
Yos 5:13

l 2Fa 19:1

m 2Sa 24:17

Safu ya 2

a Zb 51:4

b Kut 32:12
Hes 16:22

c 2Sa 24:11

d 2Sa 24:18-23
2Nya 3:1

e Hes 25:8

f Isa 28:27

yekosea;^a lakini kondoo hawa—wamefanya nini? Ee Yehova Mungu wangu, tafadhali, acha mkono wako uniadhibu mimi na nyumba ya baba yangu; lakini usiwapige watu wako.”^b

18 Ndipo malaika wa Yehova akamwambia Gadi^c amwambie Daudi apande na kumjengea Yehova madhabahu kwenye uwanja wa kupuria nafaka wa Ornani Myebusi.^d
19 Basi Daudi akapanda kulingana na neno la Gadi, alilosema kati-ka jina la Yehova.
20 Wakati huo, Ornani akageuka na kumwona huyo malaika, na wanawe wanne waliokuwa pamoja naye wakajificha. Wakati huo Ornani alikuwa akipu-ra ngano.
21 Daudi alipopanda na kufika kwake, Ornani alitazama na kumwona Daudi, mara moja akatoka kwenye uwanja wa kupuria na kumwinamia Daudi kifudufudi.
22 Daudi akamwambia Ornani: “Niuzie* uwanja wa kupuria ili nimjengee Yehova madhabahu kwenye uwanja huo. Niu-zie kwa bei kamili, ili ugonjwa hatari ambao umewakumba watu ukomeshwe.”^e
23 Lakini Ornani akamwambia Daudi: “Uchukue uwe wako, bwa-na wangu mfalme fanya lolote unaloona ni jema.* Tazama, ninatoa ng’ombe kwa ajili ya dhahabu za kuteketezwa na kifaa cha kupuria^f utakachotumia kama kuni na ngano ya toleo la nafaka. Ninatoa vitu hivi vyote.”

24 Hata hivyo, Mfalme Daudi akamwambia Ornani: “Hapana, ni lazima niunue kwa bei kamili, kwa sababu sitachukua kitu chako

21:22 *Tnn., “Nipe.” 21:23 *Tnn., “kili-cho chema machoni pako.”

21:15 *Au “kuhuzunika.”

na kumpa Yehova au kutoa dhabihu za kuteketezwa ambazo hazinigharimu chochote.”^a **25** Basi Daudi akampimia Ornani shekeli 600 za dhahabu* kwa ajili ya uwanja huo. **26** Kisha Daudi akamjengea Yehova madhabahu^b mahali hapo na kutoa dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za ushirika, akasali kwa Yehova, ambaye sasa alimjibu kwa kushusha moto^c kutoka mbinguni kwenye madhabahu hiyo ya dhabihu za kuteketezwa. **27** Kisha Yehova akamwagiza yule malaika^d aurudishe upanga wake kwenye ala. **28** Wakati huo, Daudi alipoona kwamba Yehova amemjibu kwenye uwanja wa kupuria wa Ornani Myebusi, akaendelea kutoa dhabihu hapo. **29** Hata hivyo, lile hema la ibada la Yehova ambalo Musa alikuwa ameteengeza nyikani na ile madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa vilikuwa mahali pa juu kule Gibeoni wakati huo.^e **30** Lakini Daudi hakuweza kwenda mbele yake ili kutafuta ushauri wa Mungu, kwa maana aliogopa upanga wa malaika wa Yehova.

22 Ndipo Daudi akasema: “Hii ndiyo nyumba ya Yehova Mungu wa kweli, na hii ndiyo madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa kwa ajili ya Waisraeli.”^f

2 Kisha Daudi akaagiza wakaaji wageni^g waliokuwa katika nchi ya Israeli wakusanywe, naye akawapa kazi ya kukata mawe na kuyachonga ili yatumiwe kujenga

21:25 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 21

a 2Sa 24:24, 25

b Kut 20:25

c Law 9:23, 24
1Fa 18:38
2Nya 7:1d 2Sa 24:16
Zb 103:20e 1Fa 3:4
1Nya 16:39
2Nya 1:3

SURA YA 22

f Kum 12:5, 6
2Sa 24:18
2Nya 3:1g 1Fa 9:20, 21
2Nya 2:17, 18

Safu ya 2

a 1Fa 5:15, 17
1Fa 6:7
1Fa 7:9

b 1Fa 7:47

c 2Sa 5:11

d 1Fa 5:6, 8

e 2Nya 2:3

f 1Fa 3:7

g 2Nya 2:5

h Hag 2:3

i Zb 68:29

j Kum 12:5, 6
2Sa 7:2
Zb 132:3-5

k 1Nya 17:4

l 1Nya 28:5

m 2Sa 7:12, 13
1Fa 4:25
1Fa 5:4

n 2Sa 12:24

nyumba ya Mungu wa kweli.^a **3** Daudi pia alitayarisha kiasi kikubwa sana cha chuma ili kitumiwe kutengenezea misumari ya milango ya malango na pia vibanio, na shaba nyingi sana hivi kwamba haingeweza kupimwa,^b **4** na pia mbao za mierezi^c zisizohesabika, kwa maana Wasidoni^d na Watiro^e walimletea Daudi mbao nyingi sana za mierezi. **5** Daudi akasema: “Mwanangu Sulemani ni mchanga na hana uzoefu,^{*f} na nyumba itakayojengwa kwa ajili ya Yehova itakuwa na utukufu usio na kifani,^g hivi kwamba umaarufu na umaridadi^h wake utajulikana katika nchi zote.ⁱ Kwa hiyo, nitafanya matayarisho kwa ajili yake.” Basi Daudi akatayarisha vifaa vingi sana kabla ya kifo chake.

6 Isitoshe, alimwita Sulemani mwanawe na kumwagiza amjengee nyumba Yehova Mungu wa Israeli. **7** Daudi alimwambia hivi Sulemani mwanawe: “Moyo wangu ulitamani kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wangu.^j **8** Lakini neno la Yehova lilinijia likisema, ‘Umewaga damu nyingi sana, nawe umepigana vita vikubwa. Hutajenga nyumba kwa ajili ya jina langu,^k kwa maana umemwaga damu nyingi sana duniani mbele zangu. **9** Tazama! Utazaa mwana^l atakayekuwa mtu wa amani,^{*m} nami nitampumzisha kutokana na maadui wake wote wanaomzunguka,^m kwa maana jina lake litakuwa Sulemani,ⁿ nami nitawapa

22:5 *Au “hana uwezo.” 22:9 *Tnn., “mtulivu.” ^aLinatokana na neno la Kiebrania linalomaanisha “Amani.”

Waisraeli amani na utulivu katika siku zake.^a **10** Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili ya jina langu.^b Atakuwa mwanangu, nami nitakuwa baba yake.^c Nitakiimarisha kabisa kiti cha ufalme wake juu ya Israeli milele.^d

11 “Sasa, mwanangu, Yehova na awe pamoja nawe, nawe ufanikiwe na kujenga nyumba ya Yehova Mungu wako, kama alivyosema kukuhusu wewe.^e

12 Ila tu Yehova akupe busara na uelewaji^f atakapokupa mamlaka juu ya Israeli, ili uweze kuishika sheria ya Yehova Mungu wako.^g **13** Utafanikiwa ikiwa utashika kwa uangalifu masharti^h na sheria* ambazo Yehova alimwamuru Musa awape Waisraeli.ⁱ Uwe jasiri na imara. Usiogope wala usihofu.^j **14** Tazama, nimejitahidi kabisa kufanya matayarisho kwa ajili ya nyumba ya Yehova, nimeweka talanta 100,000* za dhahabu na talanta 1,000,000 za fedha na shaba nyingi sana^k na chuma hivi kwamba haviwezi kupimwa, nami nimetayarisha mbao na mawe,^l lakini utaoengeza vitu hivyo. **15** Una wafanyakazi wengi sana—wakataji wa mawe, waashi,^m maseremala, na wafanyakazi wenye ustadi wa kila aina.ⁿ **16** Dhahabu, fedha, shaba, na chuma haviwezi kupimwa.^o Haya, anza kazi, Yehova na awe pamoja nawe.”^p

17 Kisha Daudi akawaagiza wakuu wote wa Israeli wamsaidie Sulemani mwanawe, akawaambia: **18** “Je, Yehova, Mungu wenu hayuko pa-

22:13 *Tnn., “hukumu.” 22:14 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 22

a Zb 72:7
b 1Fa 5:5
c 2Sa 7:14
Ebr 1:5
d 1Nya 17:12-14
Zb 89:35, 36
e 1Nya 28:20
f 2Nya 1:10
Zb 72:1
g Kum 4:6
h Law 19:37
1Nya 28:7
i Kum 12:1
Kum 17:18, 19
Yos 1:8
1Fa 2:3
1Nya 28:7
Zb 19:8, 11
j Yos 1:6, 9
1Nya 28:20
k 1Nya 29:6, 7
l 1Nya 29:2-4
m 1Fa 5:17
1Fa 6:7
1Fa 7:9
n 1Fa 7:13, 14
o 1Nya 22:3
p 2Nya 1:1

Safu ya 2

a Kum 4:29
2Nya 20:3
Da 9:3
b 1Fa 6:1
c 1Fa 8:6, 21
d Kum 12:21
1Fa 8:29
1Fa 9:3

SURA YA 23

e 1Fa 1:33, 39
1Nya 28:5
f Kut 29:8, 9
g Hes 3:6
h Hes 4:2, 3
i Kum 16:18
1Nya 26:29
2Nya 19:8
j 1Nya 26:12
k 1Nya 6:31, 32
l 2Nya 8:14
2Nya 31:2
m Kut 6:16

moja nanyi, na je, hajawapumzisha pande zote? Kwa maa-na aliwatia mikononi mwangu wakaaji wa nchi, na nchi ime-tiishwa mbele za Yehova na mbele ya watu wake. **19** Basi azimieni kwa moyo wenu wote na nafsi* yenu yote kumtafuta Yehova Mungu wenu,^a anzeni kujenga mahali patakatifu pa Yehova Mungu wa kweli,^b ili milelete sanduku la agano la Yehova na vyombo vitakatifu vya Mungu wa kweli^c katika nyumba iliyojengwa kwa ajili ya jina la Yehova.”^d

23 Daudi alipokuwa amezeeka na kukaribia mwisho wa maisha yake,* alimweka Sulemani mwanawe kuwa mfalme wa Israeli.^e

2 Akawakusanya wakuu wote wa Israeli, makuhani,^f na Walawi.^g **3** Walawi waliokuwa na umri wa miaka 30 na zaidi walihesabiwa,^h idadi yao, mwanamume kwa mwanamume,* ilikuwa 38,000. **4** Walawi 24,000 kati yao walikuwa wasimamizi wa kazi ya nyumba ya Yehova, na kulikuwa na maofisa na waamuzi 6,000,ⁱ **5** na walinzi 4,000 wa malango,^j na watu 4,000 walimsifu^k Yehova kwa ala ambazo Daudi alisema hivi kuzihusu: “Nilizitengeneza ili zitumiwe kumsifu Mungu.”

6 Kisha Daudi akawapanga* katika vikundi^l kulingana na wana hawa wa Lawi: Gershoni, Kohathi, na Merari.^m **7** Kutoka kwa Wagershoni: Ladani na Shimei. **8** Wana wa Ladani walikuwa Yehieli kiongozi wao,

22:19 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 23:1 *Tnn., “akiwa amezeeka na akiwa amejaa siku.” 23:3 *Tnn., “kichwa kwa kichwa.” 23:6 *Au “akawagawa.”

Zethamu, na Yoeli,^a wana watatu. **9** Wana wa Shimei walikuwa Shelomothi, Hazieli, na Harani, wana watatu. Hao walikuwa viongozi wa koo* za Ladani. **10** Na wana wa Shimei walikuwa Yahathi, Zina, Yeushi, na Beria. Hao wanne walikuwa wana wa Shimei. **11** Yahathi alikuwa kiongozi na wa pili alikuwa Ziza. Lakini kwa kuwa Yeushi na Beria hawakuwa na wana wengi, walihesabiwa kama ukoo* mmoja nao walipewa majukumu yaleyale.

12 Wana wa Kohathi walikuwa Amramu, Ishari,^b Hebroni, na Uzieli,^c wana wanne. **13** Wana wa Amramu walikuwa Haruni^d na Musa.^e Lakini Haruni alitengwa kando daima^f ili atakase Patakatifu Zaidi, yeye na wanawe, ili watoe dhabihu mbele za Yehova, wamhudumie, na kutangaza baraka katika jina lake sikuzote.^g **14** Majina ya wana wa Musa, mtu wa Mungu wa kweli, yaliorodheshwa miongoni mwa kabila la Walawi. **15** Wana wa Musa walikuwa Gershomu^h na Eliezeri.ⁱ **16** Shebueli^j alikuwa kiongozi wa wana wa Gershomu. **17** Rehabia^k alikuwa kiongozi wa wazao* wa Eliezeri; Eliezeri hakuwa na wana wengine, lakini wana wa Rehabia walikuwa wengi sana. **18** Shelomithi^l alikuwa kiongozi wa wana wa Ishari.^m **19** Wana wa Hebroni walikuwa Yeria kiongozi wao, wa pili Amaria, wa tatu Yahazieli, na wa nne Yekameamu.ⁿ **20** Wana wa Uzieli^o walikuwa Mika kiongozi wao na wa pili Ishia.

23:9, 11, 24 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 23:17 *Tnn., "wana."

SURA YA 23

a 1Nya 26:21, 22

b Kut 6:21

c Kut 6:18

d Kut 4:14

e Kut 6:20, 26

f Kut 28:1

g Law 9:22
Hes 6:23-27
Kum 21:5

h Kut 2:21, 22

i Kut 18:3, 4

j 1Nya 26:24

k 1Nya 26:25

l 1Nya 24:20, 22

m Hes 3:27

n 1Nya 24:20, 23

o Kut 6:22

Safu ya 2

a Kut 6:19

b 2Sa 7:1

c 1Fa 8:12, 13
Zb 135:21

d Hes 4:15

e Hes 3:9

f 1Fa 6:36

g Law 24:5, 6
1Nya 9:32h Kut 29:1, 2
Law 2:4

i Law 7:12

21 Wana wa Merari walikuwa Mali na Mushi.^a Wana wa Mali walikuwa Eleazari na Kishi. **22** Eleazari alikufa, lakini hakuwa na wana ila mabintu. Basi wana wa Kishi, watu wao wa ukoo,* waliwaoa. **23** Wana wa Mushi walikuwa Mali, Ederi, na Yeremothi, wana watatu.

24 Hao ndio waliokuwa wana wa Lawi kulingana na koo zao,* viongozi wa koo zao,* wale walioandikishwa na kuhesabiwa na kuorodheshwa kulingana na majina yao na ambao walitekeleza kazi ya utumishi wa nyumba ya Yehova, kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi. **25** Kwa maana Daudi alikuwa amesema hivi: "Yehova Mungu wa Israeli amewapumzisha watu wake,^b naye atakaa Yerusalemu milele.^c **26** Pia Walawi hawata-lazimika kubeba hema la ibada wala chombo chake chochote kinachotumiwa katika utumishi wa hema hilo."^d

27 Kwa maana kulingana na maagizo ya mwisho ya Daudi, Walawi wenye umri wa miaka 20 na zaidi walihesabiwa. **28** Jukumu lao lilikuwa kuwasaidia wana wa Haruni^e katika utumishi wa nyumba ya Yehova, kusimamia nyua,^f vyumba vya kulia chakula, kukitakasa kila kitu kitakatifu, na kazi yoyote iliyohitaji kufanywa katika utumishi wa nyumba ya Mungu wa kweli. **29** Waliwasaidia katika kazi ya mikate ya tabaka,^g unga laini wa toleo la nafaka, mikate myembamba isiyu na chachu,^h keki zilizookwa, unga wa kukandwa uliochanganywa,ⁱ na

23:22 *Tnn., "ndugu zao." 23:29 *Yaani, mikate ya wonyesho.

vipimo vyote vya wingi na ukubwa. **30** Walipaswa kusi-mama asubuhi baada ya asubuhi^a ili kumshukuru na kumsifu Yehova, na walipaswa kufanya hivyo jioni pia.^b **31** Walisaidia wakati wowote ambapo dhabihu za kute-ketezwa zilitolewa kwa Yehova nyakati za Sabato,^c miezi mipya,^d na wakati wa sherehe za majira,^e kulingana na idadi iliyoamriwa katika sheria kuzihusu, nao walifanya hivyo kwa ukawaida mbele za Yehova. **32** Walitimiza pia majukumu yao kuhusiana na hema la mkutano, mahali patakati-fu, na kuhusiana na ndugu zao wana wa Haruni katika utumishi wa nyumba ya Yehova.

24 Basi hivi ndivyo vilivyokuwa vikundi vya wazao wa Haruni: Wana wa Haruni walikuwa Nadabu, Abihu,^f Eleazari, na Ithamari.^g **2** Hata hivyo, Nadabu na Abihu walikufa kabla ya baba yao,^h nao hawakuwa na wana wowote; lakini Eleazariⁱ na Ithamari walielelea kutumikia wakiwa makuhani. **3** Daudi, pamoja na Sadoki^j kutoka kwa wana wa Eleazari na Ahimeleki kutoka kwa wana wa Ithamari, waliwagawa katika vikundi kulingana na mpangilio wao wa utumishi. **4** Kwa kuwa wana wa Eleazari walikuwa na viongozi wengi kuliko wana wa Ithamari, waliwagawa ifaavyo: Wana wa Eleazari walikuwa na viongozi 16 wa koo zao,^{*} na wana wa Ithamari walikuwa na viongozi 8 wa koo zao.*

5 Pia, waliwagawa kwa kura,^k kikundi kimoja pamoja

24:4, **6** *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 23

a Kut 29:39

b 1Nya 16:4, 37

c Kut 20:10

d Hes 10:10
Zb 81:3

e Kum 16:16

SURA YA 24

f Law 10:1

g Kut 6:23
Kut 28:1

h Hes 26:61

i Hes 16:39, 40

j 2Sa 8:17

k Met 16:33

Safu ya 2

a 1Fa 2:35

b 2Sa 8:17

c 2Sa 19:11
1Fa 1:5, 7

d Lu 1:5

e 2Fa 11:9
Lu 1:8, 23

f Kut 6:18

g 1Nya 23:16
1Nya 26:24

h 1Nya 23:17

i 1Nya 23:18

na kingine, kwa maana kuli-kuwa na wakuu wa mahali patakati-fu na wakuu wa Mungu wa kweli kutoka kwa wana wa Eleazari na pia wana wa Ithamari. **6** Kisha Shemaya mwana wa Nethaneli mwandishi wa Walawi akaandika majina yao mbele ya mfalme, wakuu, kuhani Sadoki,^a Ahimeleki^b mwana wa Abiathari,^c na viongozi wa koo* za makuhani na za Walawi, ukoo* mmoja ulichaguliwa kutoka kwa Eleazari na ukoo mmoja ulichaguliwa kutoka kwa Ithamari.

7 Kura ya kwanza ilimwangukia Yehoyaribu; ya pili Yedaya, **8** ya tatu Harimu, ya nne Seorimu, **9** ya tano Malkiya, ya sita Miyamini, **10** ya saba Hakozi, ya nane Abiya,^d **11** ya tisa Yeshua, ya kumi Shekania, **12** ya 11 Eliashibu, ya 12 Yakimu, **13** ya 13 Hupa, ya 14 Yeshebeabu, **14** ya 15 Bilga, ya 16 Imeri, **15** ya 17 Heziri, ya 18 Hapisesi, **16** ya 19 Pethahia, ya 20 Yehezkel, **17** ya 21 Yakini, ya 22 Gamuli, **18** ya 23 Delaya, ya 24 Maazia.

19 Huo ndio uliokuwa mpangilio wao wa utumishi^e walipokuwa wakiingia katika nyumba ya Yehova kulingana na utaratibu uliowekwa na Haruni babu yao, kama Yehova Mungu wa Israeli alivyokuwa amemwamuru.

20 Hawa ndio Walawi waliobaki: kutoka kwa wana wa Amramu^f kulikuwa na Shubaeli;^g kutoka kwa wana wa Shubaeli, Yehdeya; **21** wana wa Rehabia:^h kutoka kwa wana wa Rehabia, Ishia kiongozi wao; **22** kutoka kwa Waishari, Shelomothi;ⁱ kutoka kwa wana wa Shelomothi, Yahathi; **23** na kutoka kwa

wana wa Hebroni, Yeria^a kiongozi wao, wa pili Amaria, wa tatu Yahazieli, wa nne Yekameamu; **24** kutoka kwa wana wa Uzieli, Mika; kuto-ka kwa wana wa Mika, Shami-ri. **25** Ndugu ya Mika aliku-wa Ishia; kutoka kwa wana wa Ishia, Zekaria.

26 Wana wa Merari^b wali-kuwa Mali na Mushi; kutoka kwa wana wa Yaazia, Beno. **27** Wana wa Merari: kuto-ka kwa Yaazia, Beno, Shoha-mu, Zakuri, na Ibri; **28** kuto-ka kwa Mali, Eleazari, ambaye hakuwa na wana wowote;^c **29** Kishi: kutoka kwa wana wa Kishi, Yerahmeeli; **30** na wana wa Mushi walikuwa Mali, Ederi, na Yerimothi.

Hao ndio waliokuwa wana wa Lawi kulingana na koo zao.* **31** Na pia walipiga kura^d kama walivyofanya ndugu zao wana wa Haruni mbele ya Mfalme Daudi, Sadoki, Ahi-meleki, na viongozi wa koo* za makuhani na za Walawi. Kuhusiana na koo,* kiongozi alikuwa sawa kabisa na ndugu yake mdogo.

25 Isitoshe, Daudi na wa-kuu wa vikundi vya utu-mishi waliwatenga baadhi ya wana wa Asafu, Hemani, na Yeduthuni^e ili watoe unabii kwa kutumia vinubi, vinanda,^f na matoazi.^g Hii ndiyo orodha ya wanaume waliowekwa ras-mi kwa ajili ya utumishi huo: **2** kutoka kwa wana wa Asa-fu: Zakuri, Yosefu, Nethania, na Asharela, wana wa Asafu waliokuwa chini ya usimami-zi wa Asafu, aliyetoa unabii chini ya usimamizi wa mfal-

24:30, 31 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 24

a 1Nya 26:31

b Mwa 46:11

c 1Nya 23:22

d Met 16:33

SURA YA 25

e 1Nya 16:41, 42
2Nya 5:11, 12
2Nya 35:15

f 1Sa 10:5

g 1Nya 15:16

Safu ya 2

a 1Nya 16:41, 42

b 1Nya 15:16, 18

c Efe 5:19

d 1Nya 15:16, 19

e 1Nya 13:8
1Nya 15:16
1Nya 16:5

f Met 16:33

g 1Nya 25:1, 2

h 1Nya 25:1, 3

i 1Nya 25:1, 2

me. **3** Kutoka kwa Yeduthu-ni,^a wana wa Yeduthuni wali-kuwa: Gedalia, Zeri, Yesha-ya, Shimei, Hashabia, na Ma-tithia,^b wana sita, waliokuwa chini ya usimamizi wa Yedu-thuni baba yao, aliyetoa unabii kwa kutumia kinubi, akimshu-kuru na kumsifu Yehova.^c **4** Kutoka kwa Hemani,^d wana wa Hemani walikuwa: Bukia, Matania, Uzieli, Shebueli, Yeri-mothi, Hanania, Hanani, Elia-tha, Gidalti, Romamti-ezeri, Yoshebekasha, Malothi, Hothi-ri, na Mahaziothi. **5** Hao wote walikuwa wana wa Hema-ni, mwonaji wa mfalme kuhusiana na mambo ya Mungu wa kweli ili kumtukuza;* basi Mu-ngu wa kweli alimpa Hemani wana 14 na mabinti 3. **6** Hao wote walikuwa chini ya usima-mizi wa baba yao wakiwa wa-imbaji katika nyumba ya Yehova, wakitumia matoazi, vi-nanda, na vinubi^e kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya Mu-ngu wa kweli.

Asafu, Yeduthuni, na Hema-ni walikuwa chini ya usimami-zi wa mfalme.

7 Idadi yao pamoja na ndu-gu zao waliozoezwa kumwi-mbia Yehova, wote wakiwa sta-di, ilikuwa 288. **8** Basi walipi-ga kura^f ili kupanga zamu zao, mdogo sawa na mkubwa, mwe-nye ustadi pamoja na mwana-funzi.

9 Kura ya kwanza ilimwa-ngukia Asafu kwa ajili ya Yo-sefu,^g ya pili Gedalia^h (yeye na ndugu zake na wanawe wa-likuwa 12); **10** ya tatu Zaku-ri,ⁱ wanawe na ndugu zake, 12; **11** ya nne Izri, wanawe na ndugu zake, 12; **12** ya tano

25:5 *Tnn., "kuinua pembe yake."

Nethania,^a wanawe na ndugu zake, 12; **13** ya sita Bukia, wanawe na ndugu zake, 12; **14** ya saba Yesharela, wanawe na ndugu zake, 12; **15** ya nane Yeshaya, wanawe na ndugu zake, 12; **16** ya tisa Matania, wanawe na ndugu zake, 12; **17** ya kumi Shimei, wanawe na ndugu zake, 12; **18** ya 11 Azareli, wanawe na ndugu zake, 12; **19** ya 12 Hashabia, wanawe na ndugu zake, 12; **20** ya 13 Shubaeli,^b wanawe na ndugu zake, 12; **21** ya 14 Matithia, wanawe na ndugu zake, 12; **22** ya 15 Yeremothi, wanawe na ndugu zake, 12; **23** ya 16 Hanania, wanawe na ndugu zake, 12; **24** ya 17 Yoshebekasha, wanawe na ndugu zake, 12; **25** ya 18 Hanani, wanawe na ndugu zake, 12; **26** ya 19 Malothi, wanawe na ndugu zake, 12; **27** ya 20 Eliatha, wanawe na ndugu zake, 12; **28** ya 21 Hothiri, wanawe na ndugu zake, 12; **29** ya 22 Gidalti,^c wanawe na ndugu zake, 12; **30** ya 23 Mahaziothi,^d wanawe na ndugu zake, 12; **31** ya 24 Romamti-ezeri,^e wanawe na ndugu zake, 12.

26 Hivi ndivyo vilivyokuwa vikundi vya walenzi:^f kutoka kwa Wakora, Meshelemia^g mwana wa Kore wa wana wa Asafu. **2** Na Meshelemia alikuwa na wana: Zekaria mzaliwa wa kwanza, wa pili Yediaeli, wa tatu Zebadia, wa nne Yathnieli, **3** wa tano Elamu, wa sita Yehohani, wa saba Elieho-enai. **4** Na Obed-edomu alikuwa na wana: Shemaya mzaliwa wa kwanza, wa pili Yehozabadi, wa tatu Yoa, wa nne Sakari, wa tano Nethaneli, **5** wa sita Amieli, wa saba Isakari, na wa

SURA YA 25

a 1Nya 25:1, 2

b 1Nya 25:1, 4

c 1Nya 25:1, 4

d 1Nya 25:1, 4

e 1Nya 25:1, 4

SURA YA 26

f 1Nya 9:2, 22
2Nya 23:16, 19

g 1Nya 26:14, 19

Safu ya 2

a 1Nya 26:14, 19

b Met 16:33

nane Peulethai; kwa maana Mungu alikuwa amembariki.

6 Na Shemaya mwana wake alizaa wana waliokuwa viongozi wa koo zao,* kwa maana walikuwa wanaume hodari wenye uwezo. **7** Wana wa Shemaya walikuwa: Othni, Refaeli, Obedi, na Elzabadi; na Elihu na Semakia ndugu zake, walikuwa wanaume wenye uwezo pia. **8** Hao wote walikuwa wazao wa wana wa Obed-edomu; wao pamoja na wana wao na ndugu zao walikuwa wanaume wenye uwezo waliostahili kwa ajili ya utumishi huo, watu 62 wa Obed-edomu. **9** Na Meshelemia^a alikuwa na wana na ndugu, wanaume 18 wenye uwezo. **10** Na Hosa wa wana wa Merari alikuwa na wana. Shimri ndiye aliyekuwa kiongozi, kwa maana ingawa hakuwa mzaliwa wa kwanza, baba yake alimweka kuwa kiongozi, kwa pili Hilkia, wa tatu Tebalia, wa nne Zekaria. Wana wote wa Hosa na ndugu zake walikuwa 13.

12 Katika vikundi hivyo vya walenzi wa malango, viongozi walikuwa na kazi kama za ndugu zao, kuhudumu katika nyumba ya Yehova. **13** Kwa hiyo walipiga kura,^b mdogo sawa na mkubwa kulingana na koo zao,* kwa ajili ya malango mbalimbali. **14** Kura ya upande wa mashariki ilimwangukia Shelemia. Wakapiga kura kwa ajili ya Zekaria mwanawe, mshauri mwenye busara, aliangukiwa na kura ya upande wa kaskazini. **15** Obed-edomu alipata kura ya upande wa kusini, na

26:6, 13 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

wanawe^a walipewa kazi ya maghala. **16** Shupimu na Hosa^b walipata kura ya upande wa magharibi, karibu na Lango la Shalekethi kando ya barabara kuu inayoelekea juu, kikundi cha ulinzi karibu na kikundi kingine cha ulinzi; **17** kulikuwa na Walawi sita upande wa mashariki; wanne kila siku upande wa kaskazini, na wanne kila siku upande wa kusini; na kwenye maghala,^c wawili wawili; **18** kwa ajili ya baraza upande wa magharibi, kulikuwa na wanne kwenye barabara kuu^d na wawili barazani. **19** Hivyo ndivyo vilivyokuwa vikundi vya walinzi wa malango vya wana wa Wakora na wa Wamerari.

20 Kuhusu Walawi, Ahiya alisimamia hazina za nyumba ya Mungu wa kweli na hazina za vitu vilivyofanywa kuwa vitakatifu.*^e **21** Wana wa Ladani: wana wa Mgershoni mwana wa Ladani, viongozi wa koo* za Ladani Mgershoni, kulikuwa na Yehieli^f **22** na wana wa Yehieli, Zethamu na Yoeli ndugu yake. Walisimamia hazina za nyumba ya Yehova.^g **23** Kutoka kwa Waamramu, Waishari, Wahebroni, na Wauzieli,^h **24** Shebueli mwana wa Gershomu mwana wa Musa alikuwa kiongozi aliyesimamia maghala. **25** Na kuhusu ndugu zake, kutoka kwa Eliezeriⁱ kulikuwa na Rehabia^j mwana wa Eliezeri, Yeshaya mwana wa Rehabia, Yoramu mwana wa Yeshaya, Zikri mwana wa Yoramu, na Shelomothi mwana wa Zikri. **26** Huyu Shelomothi

26:20 *Au "vitu vilivyowekwa wakfu."
26:21, 26, 31, 32 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 26

- a 1Nya 26:4, 5
b 1Nya 26:10, 11
c 1Nya 26:15
d 1Nya 26:16
e 1Fa 7:51
1Fa 14:25, 26
1Nya 9:26
1Nya 18:10, 11
f 1Nya 29:8
g 1Fa 15:18
h Hes 3:27
i Kut 18:3, 4
j 1Nya 23:17

Safu ya 2

- a Hes 31:50
1Nya 18:10, 11
b 1Nya 29:3, 4
c 1Nya 29:6, 7
d Yos 6:19
e Hes 31:28
f 1Sa 9:9
g 1Sa 14:50
h 2Sa 20:23
i 2Sa 2:18
j 1Nya 23:12
k Kum 17:9
2Nya 19:8
l 1Nya 23:12
m 1Nya 23:19
n 1Nya 29:26, 27
o Yos 13:24, 25
Yos 21:8, 39

na ndugu zake walisimamia hazina zote za vitu vilivyofanywa kuwa vitakatifu,^a ambavyo Mfalme Daudi,^b viongozi wa koo,^{*c} wakuu wa maelfu na wa mamia, na wakuu wa jeshi walikuwa wamevifanya kuwa vitakatifu. **27** Baadhi ya vitu walivyopata vitani^d na baadhi ya nyara^e walizifanya kuwa takatifu ili kuidumisha nyumba ya Yehova; **28** pia, vitu vyote ambavyo Samweli mwonaji,^f Sauli mwana wa Kishi, Abneri^g mwana wa Neri, na Yoabu^h mwana wa Seruyaⁱ walikuwa wamevifanya kuwa vitakatifu. Kitu chochote ambacho mtu yeyote alikifanya kuwa vitakatifu kiliwekwa chini ya usimamizi wa Shelomithi na ndugu zake.

29 Kutoka kwa Waishari,^j Kenania na wanawe walipewa kazi za nje za usimamizi wa kiwa maofisa na waamuzi^k wa Israeli.

30 Kutoka kwa Wahebroni,^l Hashabia na ndugu zake, wanaume 1,700 wenye uwezo, waliwasimamia wakuu wa Israeli katika eneo lililokuwa upande wa magharibi wa Yordani kuhusiana na kazi zote za Yehova na utumishi wa mfalme. **31** Kutoka kwa Wahebroni, Yeriya^m alikuwa kiongozi wa Wahebroni kulingana na nasaba ya ukoo wao.* Katika mwaka wa 40 wa utawala wa Daudi,ⁿ walitafutwa, na wanaume hodari wenye uwezo wakapatikana miongoni mwao kule Yazeri,^o Gileadi. **32** Na ndugu zake walikuwa 2,700, wanaume wenye uwezo, viongozi wa koo.* Basi Mfalme Daudi akawaweka wawasimamie watu wa kabila la Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la

Manase, katika kila jambo la Mungu wa kweli na la mfalme.

27 Hii ndiyo idadi ya Waisraeli, viongozi wa koo,* wakuu wa maelfu na wa mama,^a na maofisa wao waliomhudumia mfalme^b katika kila jambo lililohusu vikundi ambavyo viliingia ndani na kutoka nje mwezi baada ya mwezi, miezi yote ya mwaka; kila kikundi kilikuwa na watu 24,000.

2 Msimamizi wa kikundi cha kwanza kwa ajili ya mwezi wa kwanza alikuwa Yashobeamu^c mwana wa Zabdieli, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **3** Kati ya wana wa Perezi,^d yeye ndiye aliyekuwa kiongozi wa wakuu wote wa vikundi vilivyopewa zamu ya kutumikia katika mwezi wa kwanza. **4** Msimamizi wa kikundi cha mwezi wa pili alikuwa Dodai^e Mwahohi,^f na Miklothi ndiye aliyekuwa kiongozi, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **5** Msimamizi wa kikundi cha tatu kilichopewa zamu ya kutumikia katika mwezi wa tatu alikuwa Benaya^g mwana wa Yehoyada^h mkuu wa makuhani, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **6** Huyu Benaya alikuwa shujaa hodari miongoni mwa wale 30 na ndiye aliyekuwa msimamizi wao, na kiongozi wa kikundi chake alikuwa Amizabadi mwanawe. **7** Msimamizi wa nne kwa ajili ya mwezi wa nne alikuwa Asaheli,ⁱ ndugu ya Yoabu,^j na baada yake Zebadia mwanawe, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **8** Msimamizi wa tano kwa ajili ya mwezi wa tano

27:1 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 27

a Kut 18:25
Kum 1:15
1Sa 8:11, 12

b 1Nya 28:1

c 1Nya 11:11

d Hes 26:20, 21

e 2Sa 23:9

f 1Nya 8:1, 4

g 2Sa 23:20-23
1Fa 4:4

h 1Nya 12:27

i 2Sa 2:18
2Sa 23:8, 24

j 1Nya 2:15, 16

Safu ya 2

a 2Sa 23:8, 26

b 2Nya 11:5, 6
Amo 1:1

c 1Nya 11:10, 27

d 2Sa 21:18

e Hes 26:20

f 2Sa 23:8, 27

g 1Nya 6:60, 64

h 2Sa 23:8, 28

i Hes 26:20

j 2Sa 23:8, 30

k 1Sa 16:1, 6
1Sa 17:28

alikuwa Shamhuthi Mwizrahia, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **9** Msimamizi wa sita kwa ajili ya mwezi wa sita alikuwa Ira^a mwana wa Ikeshi Mtekoa,^b na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **10** Msimamizi wa saba kwa ajili ya mwezi wa saba alikuwa Helezi^c Mpeloni kutoka kwa Waefraimu, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **11** Msimamizi wa nane kwa ajili ya mwezi wa nane alikuwa Sibekai^d Mhusha kutoka kwa Wazera,^e na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **12** Msimamizi wa tisa kwa ajili ya mwezi wa tisa alikuwa Abizeri^f Mwanathothi^g kutoka kwa Wabenjamini, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **13** Msimamizi wa kumi kwa ajili ya mwezi wa kumi alikuwa Maharai^h Mnetofa kutoka kwa Wazera,ⁱ na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **14** Msimamizi wa 11 kwa ajili ya mwezi wa 11 alikuwa Benaya^j Mpirathoni kutoka kwa wana wa Efraimu, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000. **15** Msimamizi wa 12 kwa ajili ya mwezi wa 12 alikuwa Heldai Mnetofa, wa Othnieli, na kikundi chake kilikuwa na watu 24,000.

16 Hawa ndio waliokuwa viongozi wa makabila ya Israeli: Wa kabila la Rubeni, Eliezeri mwana wa Zikri; wa kabila la Simeoni, Shefatia mwana wa Maaka; **17** wa kabila la Lawi, Hashabia mwana wa Kemueli; wa wazao wa Haruni, Sadoki; **18** wa kabila la Yuda, Elihu,^k mmoja wa ndugu za Daudi; wa kabila la Isakari, Omri mwana wa Mikaeli; **19** wa kabila la Zabulo-

ni, Ishmaya mwana wa Obadia; wa kabila la Naftali, Yerimothi mwana wa Azrieli; **20** wa kabila la Efraimu, Hoshea mwana wa Azazia; wa nusu ya kabila la Manase, Yoeli mwana wa Pedaya; **21** wa nusu ya kabila la Manase kule Gileadi, Ido mwana wa Zekaria; wa kabila la Benjamini, Yaasieli mwana wa Abneri;^a **22** wa kabila la Dani, Azareli mwana wa Yerohamu. Hao ndio waliokuwa wakuu wa makabila ya Israeli.

23 Daudi hakuwahesabu wale waliokuwa na umri wa miaka 20 kurudi chini, kwa sababu Yehova alikuwa ameahidi kwamba angewafanya Waisraeli wawe wengi kama nyota za mbinguni.^b **24** Yoabu mwana wa Seruya alikuwa ameanza kuwahesabu, lakini hakumaliza; hasira ya Mungu iliwaka dhidi ya Waisraeli kwa sababu ya jambo hilo,^c na idadi hiyo haikuandikwa katika masimulizi ya historia ya nyakati za Mfalme Daudi.

25 Azmavethi mwana wa Adieli ndiye aliyesimamia hazina za mfalme.^d Yonathani mwana wa Uzia alisimamia maghala yaliyokuwa* mashambani, katika majiji, vijijini, na katika minara. **26** Ezri mwana wa Kelubu aliwasilimamia wafanyakazi waliolima mashamba. **27** Shimei Mrama alisimamia mashamba ya mizabibu; Zabdi Mshifi alisimamia maghala ya divai iliyotengenezwa kwa zabibu zilizozalishwa katika mashamba ya mizabibu. **28** Baalhanani Mgederi alisimamia mashamba ya mizeituni na mi-

27:25 * Tnn., "hazina zilizokuwa."

SURA YA 27

a 1Sa 14:50
2Sa 3:27

b Mwa 15:5

c 2Sa 24:2, 15
1Nya 21:6, 7

d 2Fa 18:15

Safu ya 2

a 2Nya 9:27

b 2Nya 26:9, 10

c Isa 35:2

d 2Sa 13:3
2Sa 21:21

e 1Nya 3:1-9

f 2Sa 15:12
2Sa 16:23
2Sa 17:23

g 2Sa 15:37
2Sa 16:16, 17

h 2Sa 23:20-23
1Fa 2:35

i 1Fa 1:7

j 1Nya 11:6

SURA YA 28

k 1Nya 27:1

l Kut 18:25

m 1Nya 27:25, 29

n 1Nya 3:1-9

o 1Nya 11:10

kuyu^a katika Shefela;^b Yoashi alisimamia maghala ya mafuta. **29** Shitrai Msharoni alisimamia makundi ya ng'ombe yaliyolisha kule Sharoni,^c na Shafati mwana wa Adlai alisimamia makundi ya ng'ombe katika mabonde tambarare.* **30** Obili Mwishmaeli alisimamia ngamia; Yehdeya Mmeronothi alisimamia punda. **31** Yazizi Mhagri alisimamia makundi ya kondoo na mbuzi. Hao wote ndio waliokuwa wasimamizi wa mali za Mfalme Daudi.

32 Yonathani,^d mpwa wa Daudi, alikuwa mshauri, mwanamume mwenye uelewaji na pia mwandishi, na Yehieli mwana wa Hakmoni aliwatumza wana wa mfalme.^e **33** Ahithofeli^f alikuwa mshauri wa mfalme, na Hushai^g Mwarki alikuwa rafiki ya* mfalme. **34** Baada ya Ahithofeli kulikuwa na Yehoyada mwana wa Benaya^h na Abiathari;ⁱ na Yoabu^j alikuwa mkuu wa jeshi la mfalme.

28 Kisha Daudi akawakusanya Yerusalemu wakuu wote wa Israeli: wakuu wa makabila, viongozi wa vikundi^k vilivyomhudumia mfalme, wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia,^l wasimamizi wa mali zote za mfalme na mifugo yake^m na wa wanawe,ⁿ pamoja na maofisa wa makao ya mfalme na kila mwanamume hodari mwenye uwezo.^o **2** Halafu Mfalme Daudi akasimamia na kusema:

"Nisikilizeni, ndugu zangu na watu wangu. Moyo wangu ulitamani kujenga nyumba

27:29 * Tnn., "nchi tambarare za chini."

27:33 * Au "msiri wa."

ambamo sanduku la agano la Yehova lingekaa* na ambayo ingekuwa kiti cha miguu cha Mungu wetu,^a nami nilifanya matayarisho ya kuijenga.^b

3 Lakini Mungu wa kweli akaniambia, 'Hutajenga nyumba kwa ajili ya jina langu,^c kwa maana wewe ni mtu wa vita, nawe umemwaga damu.'^d

4 Hata hivyo, Yehova Mungu wa Israeli alinichagua kutoka katika nyumba yote ya baba yangu niwe mfalme wa Israeli milele,^e kwa maana alimchagua Yuda kuwa kiongozi^f na kutoka katika nyumba ya Yuda aliichagua nyumba ya baba yangu,^g na kati ya wana wa baba yangu alinikubali mimi niwe mfalme wa Israeli yote.^h **5** Na kutoka kati ya wanangu wote—kwa maana Yehova amenipa wana wengi—alimchagua Sulemani mwananguⁱ aketi kwenye kiti cha ufalme wa Yehova juu ya Israeli.^k

6 "Akaniambia, 'Sulemani mwana wako ndiye atakayejenga nyumba yangu na nyua zangu, kwa maana nimemchagua yeye kuwa mwanangu, nami nitakuwa baba yake.'^l **7** Nitauimarisha kabisa ufalme wake milele^m ikiwa atazishika kwa dhati amri zangu na sheria zangu,ⁿ kama anavyofanya sasa.'^o **8** Basi, nasema machoni pa Waisraeli wote, kutaniko la Yehova, na masikioni mwa Mungu wetu: Shikeni kwa uangalifu na mtafute amri zote za Yehova Mungu wenu, ili mwimiliki nchi nzuri^o na kuwaachia wana wenu kuwa urithi wa kudumu baada yenu.

28:2 *Tnn., "lingepumzikia." 28:7 *Tnn., "maamuzi yangu ya hukumu."

SURA YA 28

a Zb 132:3-5

b 1Nya 22:2-4

c 1Nya 17:4

d 1Nya 22:7, 8

e 1Sa 16:1, 13
2Sa 7:8
Zb 89:20f Mwa 49:10
1Nya 5:2
Zb 60:7

g Ru 4:22

h 1Sa 13:14
1Sa 16:11, 12

i 1Nya 3:1-9

j 1Nya 22:9

k 1Nya 17:14
2Nya 1:8

l 2Sa 7:13, 14

m 1Nya 17:13, 14
Zb 72:8n Kum 12:1
1Fa 6:12

o Kum 6:3

Safu ya 2

a Kum 10:12

b 1Sa 16:7
1Nya 29:17
Met 17:3
Ufu 2:23c Kum 31:21
Zb 139:2d Mt 7:7
Ebr 11:6
Yak 4:8e Kum 31:17
2Nya 15:2
Ebr 10:38

f Ebr 8:5

g 2Nya 3:4

h Law 16:2
1Fa 6:19i 1Fa 6:36
1Fa 7:12j 1Nya 9:26
1Nya 26:20

k 1Nya 24:1

l 2Nya 4:7

9 "Nawe, Sulemani mwangu, mjue Mungu wa baba yako na kumtumikia kwa moyo kamili*^a na kwa nafsi[#] yenye shangwe;^Δ kwa maana Yehova huichunguza kabisa mioyo yote,^b naye hutambua kila mwelekeo wa fikira.^c Ukitafuta, atakuruhusu umpate,^d lakini ukimwacha, atakukataa milele.^e **10** Ona kwamba Yehova amekuchagua wewe ujenge nyumba ili iwe mahali patakatifu. Uwe jasiri, anza kazi."

11 Kisha Daudi akampa Sulemani mwana wake ramani ya ujenzi^f wa ukumbi^g na ya nyumba zake, maghala yake, vyumba vyake vya darini, vyumba vyake vya ndani, na nyumba ya kifuniko cha upatanisho.*^h **12** Alimpa ramani ya kila kitu alichambiwa kupitia mwongozo wa roho kuhusu ujenzi wa nyuaⁱ za nyumba ya Yehova, vyumba vyote vya kulia chakula vilivyozunguka, hazina za nyumba ya Mungu wa kweli, na hazina za vitu vilivyofanywa kuwa vitakatifu;*^j **13** pia kuhusu vikundi vya makuhani^k na Walawi, kuhusu kazi zote za utumishi wa nyumba ya Yehova, na kuhusu vyombo vyote vya utumishi wa nyumba ya Yehova; **14** pia kuhusu uzito wa dhahabu, dhahabu ya vyombo vyote vya utumishi mbalimbali, uzito wa vyombo vyote vya fedha, na vyombo vyote vya utumishi mbalimbali; **15** pia uzito wa vinara vya taa vya dhahabu/

28:9 *Au "wenye ujitoaji kamili." #Angalia Kamusi, uku. 2012. ΔAu "kwa hiari." 28:11 *Au "nyumba ya kufunika dhambi." 28:12 *Au "vilivyowekwa wakfu."

na taa zake za dhahabu, uzito wa vinara mbalimbali vya taa na taa zake, na uzito wa vinara vya taa vya fedha, uzito wa kila kinara cha taa na taa zake kulingana na matumizi yake; **16** pia kuhusu uzito wa dhahabu za meza za mikate ya tabaka,^a uzito wa kila meza, na pia fedha kwa ajili ya meza za fedha, **17** kuhusu nyuma,^{*} mabakuli, magudulia ya dhahabu safi, na uzito wa mabakuli madogo ya dhahabu,^b uzito wa kila bakuli dogo, na uzito wa mabakuli madogo ya fedha, uzito wa kila bakuli dogo. **18** Pia alimpa uzito wa dhahabu safi kwa ajili ya madhabahu ya uvumba^c na kwa ajili ya mfano wa lile gari,^d yaani, wale makerubi^e wa dhahabu walioyoosha mabawa yao na kulifunika sanduku la agano la Yehova. **19** Daudi akasema: “Mkono wa Yehova ulikuwa juu yangu, naye alinipa ufahamu wa kuandika^f mambo yote kuhusu ramani hii ya ujenzi.”^g

20 Kisha Daudi akamwambia Sulemani mwanawe: “Uwe jasiri na imara na uanze kazi. Usiogope wala usihofu, kwa maana Yehova Mungu, Mungu wangu, yuko pamoja nawe.^h Hatakuacha wala kukutupa,ⁱ lakini atakuwa pamoja nawe mpaka kazi yote ya utumishi wa nyumba ya Yehova itakapokamilika. **21** Na hivi ndivyo vikundi vya makuhani/ na vya Walawi^k kwa ajili ya utumishi wote wa nyumba ya Mungu wa kweli. Una wafanyakazi walio tayari, na wenyewe ustadi wa kufanya utumishi wa kila aina,^l na pia wa-

28:16 *Yaani, mikate ya wonyesho.
28:17 *Wingi wa kifaa kinachoitwa uma.

SURA YA 28

a 2Nya 4:8, 19

b 1Fa 7:48, 50

c 1Fa 7:48

d Zb 18:10

e Kut 25:20
1Sa 4:4
1Fa 6:23

f Kut 25:9, 40

g 1Nya 28:11

h Kum 31:6
Yos 1:6, 9
Ro 8:31

i Yos 1:5

j 1Nya 24:1

k 1Nya 24:20

l Kut 36:1, 2

Safu ya 2

a 1Nya 22:17
1Nya 28:1

SURA YA 29

b 1Nya 28:5

c 1Fa 3:7

d 2Nya 2:4

e 1Nya 22:3, 16

f 1Nya 22:4, 14

g Zb 26:8
Zb 27:4
Zb 122:1

h 1Nya 21:24

i Ayu 28:16

j Kut 35:5

kuu^a na watu wote watakaotekeleza maagizo yako yote.”

29 Sasa Mfalme Daudi aka-liambia kutaniko lote: “Mwanangu Sulemani, ambaye Mungu amemchagua^b ni mchanga na hana uzoefu,^{*c} na kazi hii ni kubwa, kwa maana si hekalu[#] kwa ajili ya mwanadamu, bali ni kwa ajili ya Yehova Mungu.^d **2** Nami nimejitahidi kabisa kufanya matayarisho kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu, nimetoa dhahabu ya kutengenezea vitu vya dhahabu, fedha ya kutengenezea vitu vya fedha, shaba ya kutengenezea vitu vya shaba, chuma kwa ajili ya vitu vya chuma,^e mbao^f za kutengenezea vitu vya mbao, mawe ya shohamu, na vito vinavyoonganishwa kwa saruji, na vijawe maridadi vya mvingo, kila aina ya mawe yenye thamani, na mawe mengi sana ya alabasta. **3** Isitoshe, kwa sababu ninaipenda nyumba ya Mungu wangu,^g ninatoa pia hazina yangu binafsi^h ya dhahabu na fedha kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu, pamoja na vitu vyote nilivyotayarisha kwa ajili ya nyumba hiyo takatifu, **4** na pia talanta 3,000* za dhahabu ya Ofiriⁱ na talanta 7,000 za fedha iliyosafishwa, ili zitumiwe kufunika kuta za nyumba, **5** dhahabu ya kutengenezea vitu vya dhahabu na fedha ya kutengenezea vitu vya fedha, na kwa ajili ya kazi yote itakayofanywa na mafundi. Basi ni nani anayejitolea kuja leo akiwa na zawadi mkononi kwa ajili ya Yehova?”^j

29:1 *Au “hana uwezo.” #Au “ngome; jumba la mfalme.” **29:4** *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

6 Basi wakuu wa koo,* wakuu wa makabila ya Israeli, wakuu wa maelfu na wa mamia,^a na wakuu wa kazi za mfalme^b wakajitolea kwa hiari. 7 Nao wakatoa kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya Mungu wa kweli: talanta 5,000 za dhahabu, dariki 10,000,* talanta 10,000 za fedha, talanta 18,000 za shaba, na talanta 100,000 za chuma. 8 Mtu yeyote aliyekuwa na mawe yenye thamani aliyatoa kwa ajili ya hazina ya nyumba ya Yehova, chini ya usimamizi wa Yehieli^c Mgershoni.^d 9 Watu walishangilia kwa sababu walitoa matoleo hayo ya hiari, kwa maana walimtolea Yehova matoleo hayo ya hiari kwa moyo kamili,^e na Mfalme Daudi pia alishangilia sana.

10 Kisha Daudi akamsifu Yehova mbele ya kutaniko lote. Daudi akasema: “Na usifiwe, Ee Yehova Mungu wa Israeli baba yetu, kwa umilele wote.* 11 Ee Yehova, ukuu ni wako^f na nguvu^g na uzuri na fahari na utukufu,^h kwa maana kila kitu mbinguni na duniani ni chako.ⁱ Ufalme ni wako, Ee Yehova.^j Wewe Ndiye unayejikweza mwenyewe ukiwa mkuu^u juu ya vyote. 12 Utajiri na utukufu hutoka kwako,^k nawe hutawala kila kitu,^l na mkononi mwako mna nguvu^m na uwezo,ⁿ na mkono wako unaweza kumfanya mtu awe mkuu^o na unaweza kuwapa wote nguvu.^p 13 Na sasa, Ee Mungu wetu, tunaku-

29:6 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 29:7 *Dariki ilikuwa sarafu ya dhahabu ya Waajemi. Angalia Nyongeza B14. 29:10 *Au “milele na milele.” 29:11 *Au “adhama.” *Tnn., “kichwa.”

SURA YA 29

a Kut 18:25

b 1Nya 27:25, 29
1Nya 27:31

c 1Nya 26:22

d 1Nya 6:1

e 2Ko 9:7

f Zb 145:3
1Ti 1:17

g Ufu 5:13

h 1Nya 16:27
Zb 8:1i Zb 24:1
Isa 42:5j Zb 103:19
Mt 6:10k Kum 8:18
Met 10:22
Flp 4:19

l 2Nya 20:6

m Isa 40:26

n Kum 3:24
Efe 1:19
Ufu 15:3

o 2Nya 1:11, 12

p 2Nya 16:9
Zb 18:32
Isa 40:29

Safu ya 2

a Law 25:23
Ebr 11:13b Ayu 14:1, 2
Yak 4:13, 14

c 1Nya 28:9

d Met 11:20
Met 15:8
Ebr 1:9e Zb 10:17
Zb 86:11

f Mk 12:30

g 1Fa 6:12

h 1Nya 22:14

shukuru na kulisifu jina lako linalovutia.

14 “Lakini, mimi ni nani na watu wangu ni nani hivi kwamba tukutolee matoleo haya ya hiari? Kwa maana kila kitu kinatoka kwako, nasi tumekupa vitu vinavyotoka mkononi mwako mwenyewe. 15 Kwa maana sisi ni wakaaji wage-ni mbele zako na wahamiaji, kama walivyokuwa mababu zetu wote.^a Kwa kuwa siku zetu duniani ni kama kivuli^b—hatuna tumaini. 16 Ee Yehova Mungu wetu, utajiri huu wote ambao tumetayarisha ili kukujengea nyumba kwa ajili ya jina lako takatifu unatoka mkononi mwako mwenyewe, wote ni mali yako. 17 Ee Mungu wangu, najua vizuri kwamba wewe huuchunguza moyo,^c na kwamba unapendezwa na utimilifu.*^d Kwa unyoofu wa moyo wangu, nimetoa kwa hiari vitu hivi vyote, nami nimefurikwa na shangwe kuwaona watu wako walio hapa wakikutolea matoleo ya hiari. 18 Ee Yehova, Mungu wa Abrahamu, Isaka, na Israeli, mababu zetu, idumisha mielekeo hii na fikira hizi katika mioyo ya watu wako milele, na uielekeze mioyo yao kwako.^e 19 Mpe mwanangu Sulemani moyo kamili,^f ili ashike amri zako, vikumbusho vyako,^g na masharti yako na kufanya mambo haya yote na kujenga hekalu^h ambalo nime-lifanyia matayarisho.”^h

20 Kisha Daudi akaliambia kutaniko lote: “Sasa msifuni Yehova Mungu wenu.” Na ku-

29:17 *Au “hali ya kutokuwa na lawama; unyoofu.” 29:19 *Au “wenye uji-toaji kamili.” *Au “ngome au jumba la mfalme.”

taniko lote likamsifu Yehova Mungu wa mababu zao, wakainama chini na kumsujudia Yehova na mfalme. **21** Nao wakaendelea kumtolea Yehova dhabihu na kumtolea Yehova dhabihu za kuteketezwa^a siku iliyofuata, ng'ombe dume wachanga 1,000, kondoo dume 1,000, wanakondoo dume 1,000, na matoleo yake ya vinywaji;^b walitoa dhabihu nyingi sana kwa ajili ya Waisraeli wote.^c **22** Wakaeendelea kula na kunywa mbele za Yehova siku hiyo kwa shangwe nyingi,^d nao wakamweka Sulemani mwana wa Daudi kuwa mfalme kwa mara ya pili na kumtia mafuta mbele za Yehova ili awe kiongozi,^e na pia Sadoki kuwa kuhani.^f **23** Na Sulemani akaketi kwenye kiti cha ufalme cha Yehova^g akiwa mfalme baada ya Daudi baba yake, akafanikiwa, na Waisraeli wote walimtii. **24** Wakuu wote,^h mashujaa wote hodari,ⁱ na pia wana wote wa Mfalme Dau-

SURA YA 29

- a Law 1:3
 b Law 23:12, 13
 Hes 15:5
 c 1Fa 8:63, 64
 d Kum 12:7
 2Nya 7:10
 Ne 8:12
 e 1Fa 1:38–40
 1Nya 23:1
 f 1Fa 2:35
 g 1Nya 28:5
 h 1Nya 22:17
 i 1Nya 28:1

Safu ya 2

- a 1Nya 3:1–9
 b 1Fa 3:12
 2Nya 1:1, 12
 Mhu 2:9
 c 2Sa 2:11
 d 2Sa 5:4, 5
 e 1Fa 1:1
 f 1Fa 2:10–12
 g 2Sa 7:2
 2Sa 12:1
 h 1Nya 21:9, 10

di^a wakajitiisha wenyewe chini ya Mfalme Sulemani. **25** Na Yehova akamfanya Sulemani kuwa mkuu sana machoni pa Waisraeli wote na kumpa fahari ya kifalme ambayo hakuna mfalme yeyote wa Israeli aliye-wahi kuwa nayo kabla yake.^b

26 Kwa hiyo Daudi mwana wa Yese alitawala Israeli yote, **27** alitawala Israeli kwa miaka 40. Alitawala huko Hebroni kwa miaka 7,^c na Yerusalemu kwa miaka 33.^d **28** Naye akafa akiwa amezeeka kabisa;^e aliishi maisha marefu yenye kuridhisha, akiwa na utajiri, na utukufu; na Sulemani mwanawe akawa mfalme baada yake.^f **29** Historia ya Mfalme Daudi, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, imeandikwa katika maandishi ya mwonaji Samweli, nabii Nathani,^g na mwonaji Gadi,^h **30** pamoja na utawala wake wote, ukuu wake, na matukio yanayohusu nyakati zake na nyakati za Israeli na falme zote zilizo-mzunguka.

KITABU CHA PILI CHA

MAMBO YA NYAKATI

YALIYOMO

- Sulemani aomba hekima (1-12)
Utajiri wa Sulemani (13-17)
- Matayarisho ya kujenga hekalu (1-18)
- Sulemani aanza kujenga hekalu (1-7)
Patakatifu Zaidi (8-14)
Nguzo mbili za shaba (15-17)
- Madhabahu, Bahari, na mabeseni (1-6)
Vinara vya taa, meza, na nyua (7-11a)

- Vyombo vyote vya hekalu vyakamilishwa (11b-22)
- Matayarisho ya kuzindua hekalu (1-14)
Sanduku la agano laletwa hekaluni (2-10)
- Hotuba ya Sulemani (1-11)
Sala ya Sulemani ya kuzindua hekalu (12-42)
- Hekalu lajaa utukufu wa Yehova (1-3)

- Sherehe za kuzindua hekalu (4-10)
Yehova amtokea Sulemani (11-22)
- 8 Miradi mingine ya ujenzi ya Sulemani (1-11)
Ibada ya hekaluni yapangwa (12-16)
Meli za Sulemani (17, 18)
- 9 Malkia wa Sheba amtembelea Sulemani (1-12)
Utajiri wa Sulemani (13-28)
Kifo cha Sulemani (29-31)
- 10 Waisraeli wamwasi Rehoboamu (1-19)
- 11 Utawala wa Rehoboamu (1-12)
Walawi washikamanifu wahamia Yuda (13-17)
Familia ya Rehoboamu (18-23)
- 12 Shishaki ashambulia Yerusalemu (1-12)
Mwisho wa utawala wa Rehoboamu (13-16)
- 13 Abiya, mfalme wa Yuda (1-22)
Abiya amshinda Yeroboamu (3-20)
- 14 Kifo cha Abiya (1)
Asa, mfalme wa Yuda (2-8)
Asa awashinda Waethiopia 1,000,000 (9-15)
- 15 Mabadiliko yaliyofanywa na Asa (1-19)
- 16 Asa afanya mkataba na Siria (1-6)
Hanani amkemea Asa (7-10)
Kifo cha Asa (11-14)
- 17 Yehoshafati, mfalme wa Yuda (1-6)
Kampeni ya kufundisha (7-9)
Nguvu za kijeshi za Yehoshafati (10-19)
- 18 Yehoshafati aangana na Ahabu (1-11)
Mikaya atabiri kwamba watashindwa (12-27)
Ahabu auawa Ramoth-gileadi (28-34)
- 19 Yehu amkemea Yehoshafati (1-3)
Mabadiliko yaliyofanywa na Yehoshafati (4-11)
- 20 Mataifa jirani yawatisha watu wa Yuda (1-4)
Yehoshafati asali apate msaada (5-13)
Jibu la Yehova (14-19)
Watu wa Yuda waokolewa kimuujiza (20-30)
Mwisho wa utawala wa Yehoshafati (31-37)
- 21 Yehoram, mfalme wa Yuda (1-11)
Barua kutoka kwa Eliya (12-15)
Mwisho mbaya wa Yehoram (16-20)
- 22 Ahazia, mfalme wa Yuda (1-9)
Athalia anyakua ufalme (10-12)
- 23 Yehoyada aingilia kati; Yehoashi awekwa kuwa mfalme (1-11)
Athalia auawa (12-15)
Mabadiliko yaliyofanywa na Yehoyada (16-21)
- 24 Utawala wa Yehoashi (1-3)
Yehoashi arekebisha hekalu (4-14)
Uasi imani wa Yehoashi (15-22)
Yehoashi auawa (23-27)
- 25 Amazia, mfalme wa Yuda (1-4)
Apigana vita na Edomu (5-13)
Amazia aabudu sanamu (14-16)
Apigana vita na Mfalme Yehoashi wa Israeli (17-24)
Kifo cha Amazia (25-28)
- 26 Uzia, mfalme wa Yuda (1-5)
Kampeni za kivita za Uzia (6-15)
Uzia mwenye kiburi apigwa na ukoma (16-21)
Kifo cha Uzia (22, 23)
- 27 Yothamu, mfalme wa Yuda (1-9)
- 28 Ahazi, mfalme wa Yuda (1-4)
Ashindwa na Wasiria na Waisraeli (5-8)
Odedi awaonya Waisraeli (9-15)
Watu wa Yuda wanyenyekezwa (16-19)
Ahazi aabudu sanamu; kifo chake (20-27)
- 29 Hezekia, mfalme wa Yuda (1, 2)
Mabadiliko yaliyofanywa na Hezekia (3-11)
Hekalu latakaswa (12-19)
Utumishi wa hekaluni waanzishwa tena (20-36)
- 30 Hezekia aadhimisha Pasaka (1-27)
- 31 Hezekia aung'oa uasi imani (1)
Makuhani na Walawi wategemezwa ifaavyo (2-21)
- 32 Senakeribu alitishia jiji la Yerusalemu (1-8)
Senakeribu ampinga Yehova (9-19)
Malaika aangamiza jeshi la Ashuru (20-23)
Ugonjwa wa Hezekia na kiburi chake (24-26)
Mambo aliyotimiza Hezekia na kifo chake (27-33)
- 33 Manase, mfalme wa Yuda (1-9)
Manase atubu uovu wake (10-17)

Kifo cha Manase (18-20)
Amoni, mfalme wa Yuda (21-25)

- 34 Yosia, mfalme wa Yuda (1, 2)
Mabadiliko yaliyofanywa na Yosia (3-13)
Kitabu cha Sheria chapatikana (14-21)
Unabii wa Hulda kuhusu msiba (22-28)
Yosia awasomea watu kitabu
kilichopatikana (29-33)

- 35 Yosia apanga Pasaka kubwa (1-19)
Farao Neko amuuua Yosia (20-27)
- 36 Yehoahazi, mfalme wa Yuda (1-3)
Yehoyakimu, mfalme wa Yuda (4-8)
Yehoyakini, mfalme wa Yuda (9, 10)
Sedekia, mfalme wa Yuda (11-14)
Uharibifu wa Yerusalemu (15-21)
Koreshi aagiza hekalu lijengwe
upya (22, 23)

1 Sulemani mwana wa Daudi alizidi kuimarika kati ka utawala wake, na Yehova Mungu wake alikuwa pamoja naye, akamfanya kuwa mkuu sana.^a

2 Sulemani aliagiza Waisraeli wote wakusanywe, wakuu wa maelfu na wa mamia, waamuzi, na viongozi wote wa Israeli, viongozi wa koo.*

3 Kisha Sulemani na Waisraeli wote wakaenda mahali pa juu kule Gibeoni,^b kwa maana hema la mkutano la Mungu wa kweli lilikuwa huko, hema ambalo Musa mtumishi wa Yehova alitengeneza nyikani.

4 Hata hivyo, Daudi alikuwa amelipandisha Sanduku la Mungu wa kweli kutoka Kiriath-yearimu^c na kulileta mahali ambapo Daudi alikuwa ametayarisha kwa ajili yake; alikuwa amepiga hema kwa ajili ya Sanduku hilo huko Yerusalemu.^d **5** Na ile madhabahu ya shaba^e ambayo Bezaleli^f mwana wa Uri mwana wa Huru alikuwa ametengeneza ilikuwa imewekwa mbele ya hema la ibada la Yehova; na Sulemani na Waisraeli wote walikuwa wakisali mbele yake.*

1:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.
1:5 *Au "walikuwa wakitafuta ushauri Wake hapo."

SURA YA 1

a 1Nya 29:25
Mhu 2:9
Mt 6:28, 29
Mt 12:42

b 1Fa 3:4
1Nya 21:29

c 1Nya 13:5

d 1Nya 16:1

e Kut 38:1, 2

f Kut 31:2-5

Safu ya 2

a 1Fa 3:4

b 1Fa 3:5-9

c 2Sa 7:8

d 1Nya 28:5
Zb 89:28, 29

e 2Sa 7:12
1Nya 28:6
Zb 132:11

f Mwa 13:14, 16

g Met 2:6
Yak 1:5

h Zb 72:1, 2

6 Kisha Sulemani akamtolea Yehova dhabihu mahali hapo, alitoa dhabihu 1,000 za kuteketezwa kwenye madhabahu ya shaba^a ya hema la mkutano.

7 Usiku huo Mungu akamtokea Sulemani na kumwambia: "Niombe unachotaka nikupe."^b **8** Basi Sulemani akamwambia Mungu: "Umemte ndea Daudi^c baba yangu kwa upendo mwingi mshikamani fu, nawe umeniweka kuwa mfalme baada yake.^d **9** Sasa, Ee Yehova Mungu, ahadi uliyo mpa Daudi baba yangu na ithibitike kuwa ya uaminifu,^e kwa maana umeniweka kuwa mfalme juu ya watu wengi sana kama chembe za mavumbi ya dunia.^f **10** Sasa nipe hekima na ujuzi^g ili niwaongoze watu hawa,* kwa maana ni nani anayeweza kulihukumumu taifa hili lako lililo kubwa?"^h

11 Kisha Mungu akamwambia Sulemani: "Kwa sababu moyo wako unatamani jambo hilo, nawe hukuomba mali, utajiri, wala heshima wala hukuomba wale wanaokuchukia wafe, wala hukuomba maisha marefu,* lakini umeomba hekima na ujuzi ili uwahukumumu

1:10 *Tnn., "nitoke nje mbele ya watu hawa na kurudi ndani." 1:11 *Tnn., "siku nyingi."

watu wangu ambao nimekuweka uwe mfalme wao,^a **12** nitakupa hekima na ujuzi; lakini nitakupa pia mali na utajiri na heshima, kuliko mfalme yeyote kabla yako na mfalme yeyote baada yako.”^b

13 Basi Sulemani akatoka mahali pa juu huko Gibeoni,^c kutoka mbele ya hema la mkutano, akaja Yerusalemu; naye akatawala Israeli. **14** Sulemani akaendelea kukusanya magari ya vita na farasi;* akawa na magari 1,400 ya vita na farasi* 12,000,^d naye aliwaweka katika majiji ya magari ya vita^e karibu naye huko Yerusalemu.^f **15** Mfalme alifanya fedha na dhahabu huko Yerusalemu iwe nyingi kama mawe,^g na mbao za mιεrezi ziwe nyingi kama mikuyu katika Shefela.^h **16** Farasi wa Sulemani waliletwa kutoka Misri,ⁱ na wafanyabiashara wa mfalme walinunua maku ndi ya farasi* kwa bei moja.^j **17** Kila gari kutoka Misri liliunuliwa kwa vipande 600 vya fedha, na farasi alinunuliwa kwa vipande 150; kisha waliwauzia wafalme wote wa Wahiti na wafalme wa Siria.

2 Basi Sulemani akaagiza nyumba ijengwe kwa ajili ya jina la Yehova^k na nyumba* kwa ajili ya ufalme wake.^l **2** Sulemani akawaandikisha wanaume 70,000 kuwa vibarua,* wanaume 80,000 kuwa wakataji wa mawe milimani,^m na wanaume 3,600 kuwa waangalizi wao.ⁿ **3** Pia, Sulema-

1:14 *Au “wapanda farasi.” 1:16 *Au labda, “kutoka Misri na kutoka Kue; wafanyabiashara wa mfalme waliwanunua kutoka Kue,” huenda ni Kilikia. 2:1 *Au “jumba la mfalme.” 2:2 *Au “wabeba mizigo.”

SURA YA 1

a 1Fa 3:10-13
1Fa 3:28

b 1Nya 29:25
2Nya 9:22
Mhu 2:9

c 1Fa 3:4

d Kum 17:16
1Fa 4:26

e 2Nya 8:5, 6

f 2Nya 9:25

g 1Fa 10:21

h 1Fa 10:27
2Nya 9:27

i 2Nya 9:28

j 1Fa 10:28, 29

SURA YA 2

k Kum 12:11
1Nya 22:10

l 1Fa 7:1

m 1Fa 5:15

n 1Fa 5:16
1Fa 9:22
2Nya 2:17, 18

Safu ya 2

a 1Fa 5:1

b 2Sa 5:11

c Kut 30:7

d Kut 25:30

e Hes 28:4

f Hes 28:9

g Hes 28:11

h Kum 16:16

i 1Fa 8:27
Isa 66:1
Mdo 17:24

j 1Fa 7:13, 14

k 1Nya 22:15

l 1Fa 5:6, 8
2Nya 3:5

m 1Fa 10:11

n 1Fa 5:9

ni akamtumia Hiram^a mfalme wa Tiro ujumbe huu: “Nifanyie kama ulivyomfanyia Daudi baba yangu ulipomletea mbao za mιεrezi ili ajenge nyumba ya* kuishi.^b **4** Sasa ninajenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wangu, ili niitakase kwake, nifukize uvumba wenye manukato^c mbele zake, na pia kwa ajili ya mikate ya tabaka* inayotolewa daima^d na pia dhabihu za kuteketezwa, asubuhi na jioni,^e nyakati za Sabato,^f miezi mipya,^g na kwenye majira ya sherehe^h za Yehova Mungu wetu. Huu ni wajibu wa kudumu kwa Waisraeli. **5** Nyumba nitakayojenga itakuwa kuu, kwa maana Mungu wetu ni mkuu kuliko miungu mingine yote. **6** Na ni nani anayeweza kumjengea nyumba? Kwa maana mbingu na mbingu za mbingu haziwezi kumtoshia,ⁱ basi mimi ni nani hivi kwamba nimjengee nyumba isipokuwa iwe mahali pa kufukizia moshi wa dhabihu mbele zake? **7** Sasa nilee fondi aliye na ustadi wa kutengeneza vitu kwa kutumia dhahabu, fedha, shaba,^j chuma, safu ya zambarau, nyuzi nyekundu, na nyuzi za bluu, na ambaye anajua kuchonga. Atafanya kazi Yuda na Yerusalemu pamoja na mafundi wangu stadi, ambao Daudi baba yangu aliwachagua.^k **8** Nawe uniletee mbao za mιεrezi, miberoshi,^l na misandali^m kutoka Lebanoni, kwa maana najua vizuri kwamba watumishi wako wana uzoefu wa kukata miti ya Lebanoni.ⁿ Watumishi wangu watafanya kazi pamoja na

2:3 *Au “jumba la mfalme la.” 2:4 *Yaani, mikate ya wonyesho.

watumishi wako^a **9** ili wani-tayarishie mbao nyingi sana, kwa maana nyumba nitakayo-jenga itakuwa na ukuu usio wa kawaida. **10** Sasa tazama! Nitawaletea chakula watumishi wako,^b yaani, wapasua mbao wanaokata miti: nitawaletea kori 20,000 za ngano, kori 20,000* za shayiri, bathi 20,000 za divai, na bathi 20,000[#] za mafuta.”

11 Ndipo Hiram mfalme wa Tiro akatuma barua hii kwa Sulemani: “Kwa sababu Yehova anawapenda watu wake, amekuwa kuwa mfalme wao.” **12** Kisha Hiram akasema: “Na asifiwe Yehova Mungu wa Israeli, aliyeziumba mbingu na dunia, kwa sababu amempa Mfalme Daudi mwana mwenye hekima,^c aliyebarikiwa kuwa na busara na uelwaji,^d atakayejenga nyumba kwa ajili ya Yehova na nyumba kwa ajili ya ufalme wake. **13** Sasa namtuma fundi stadi, aliyebarikiwa kuwa na uelwaji, Hiram-abi,^e **14** mwana wa mwanamke wa kabila la Dani, lakini baba yake alikuwa Mtiro; ana uzoefu wa kutengeneza vitu kwa kutumia dhahabu, fedha, shaba, chuma, mawe, mbao, sufu ya zambarau, nyuzi za bluu, kitamba bora, na nyuzi nyekundu.^f Anaweza kuchonga michongo ya kila aina na kubuni na kutengeneza kitu chochote anachoambiwa.^g Atafanya kazi pamoja na mafundi wako stadi na mafundi stadi wa bwana wangu Daudi baba yako. **15** Sasa bwana wangu tutu-

2:10 *Kori moja ilikuwa sawa na lita 220 (kilogramu 170 hivi). Angalia Nyongeza B14. [#]Bathi ilikuwa sawa na lita 22. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 2

a 1Fa 5:14

b 1Fa 5:11

c 1Fa 5:7

d 2Nya 1:11, 12

e 1Fa 7:13, 14
2Nya 4:11-16

f 2Nya 3:14

g Kut 31:2-5

Safu ya 2

a 2Nya 2:10

b 1Fa 5:6, 8

c Yos 19:46, 48
Ezr 3:7

d 1Fa 5:9

e 2Nya 8:7, 8

f 1Nya 22:2

g 1Fa 5:17, 18
1Nya 22:15

h 1Fa 5:15, 16

SURA YA 3

i 1Fa 6:1
1Fa 6:37

j Mwa 22:2, 14

k 2Sa 24:25
1Nya 21:18l 2Sa 24:18
1Nya 21:22

m 1Fa 6:2

mie ngano, shayiri, mafuta, na divai uliyotuahidi sisi watumishi wako.^a **16** Nasi tutakata miti kutoka Lebanoni,^b idadi yoyote unayohitaji, nasi tutakuletea magogo hayo yakiwa mafungu-mafungu ili yaelee baharini mpaka Yopa;^c nawe utayapeleka Yerusalemu.”^d

17 Kisha Sulemani akawahesabu wanaume wote walio-kuwa wakaaji wageni katika nchi ya Israeli,^e baada ya ile hesabu ya watu ambayo Daudi baba yake alikuwa amechukua,^f wakapatikana wanaume 153,600. **18** Kwa hiyo akawaweka watu 70,000 kati ya yao kuwa vibarua,* 80,000 kuwa wakataji wa mawe^g milimani, na 3,600 kuwa waangalizi wa kuhakikisha kwamba watu wanafanya kazi.^h

3 Kisha Sulemani akaanza kujenga nyumba ya Yehovaⁱ huko Yerusalemu juu ya Mlima Moria,^j mahali ambapo Yehova alikuwa amemtokea Daudi baba yake,^k mahali ambapo Daudi alikuwa ametayarisha kwenye uwanja wa kupuria wa Ornani Myebusi.^l **2** Alianza kujenga siku ya pili ya mwezi wa pili, katika mwaka wa nne wa utawala wake. **3** Na msingi ambao Sulemani aliweka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mungu wa kweli ulikuwa na urefu wa mikono 60 na upana wa mikono 20,^m kulingana na kipimo cha awali.* **4** Ukumbi

2:18 *Au “wabeba mizigo.” **3:3** *Kipimo cha kawaida cha mkono mmoja kilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5), lakini baadhi ya watu wanahisi kwamba “kipimo cha awali” kinarejelea kipimo cha mkono mrefu ambacho kilingana na sentimita 51.8 (inchi 20.4). Angalia Nyongeza B14.

wa mbele ulikuwa na urefu wa mikono 20, nao ulilingana na upana wa nyumba,* na kimo chake kilikuwa mikono 20;[#] naye akafunika upande wa ndani kwa dhahabu safi.^a **5** Alifunika nyumba kuu kwa mbao za miberoshi, kisha akaifunika kwa dhahabu bora,^b halafu akaipamba kwa michongo ya mitende^c na minyororo.^d **6** Pia, aliifunika nyumba hiyo kwa mawe maridadi yenye thamani;^e na dhahabu^f aliyotumia ilikuwa dhahabu kutoka Parvaimu. **7** Aliifunika nyumba, maboriti, vizingiti, kuta zake, na milango yake kwa dhahabu;^g naye akachonga makerubi kwenye kuta zake.^h

8 Kisha akajenga chumba cha Patakatifu Zaidi;^{*i} urefu wake ulilingana na upana wa nyumba, mikono 20, na upana wake ulikuwa mikono 20. Akaifunika kwa talanta 600[#] za dhahabu bora.^j **9** Uzito wa dhahabu iliyotumiwa kutengezeza misumari ulikuwa shekeli 50;^{*} naye alifunika vyumba vya darini kwa dhahabu.

10 Kisha akatengeneza mifano ya makerubi wawili katika chumba cha Patakatifu Zaidi,^{*} akawafunika kwa dhahabu.^k **11** Kwa ujumla mabawa ya makerubi hao' yalikuwa na urefu wa mikono 20; bawa moja la kerubi wa kwanza lilikuwa na urefu wa miko-

3:4 *Au "mikono 20 kufikia upana wa nyumba." #Hati fulani za kale zinasema "120," ilhali hati nyingine na tafsiri fulani zinasema "mikono 20." 3:8, 10 *Tnn., "nyumba." 3:8 #Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. 3:9 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 3

a 1Fa 6:3

b 1Fa 6:15, 22

c 1Fa 6:29

d 1Fa 6:21

e 1Nya 29:2, 8

f 1Nya 29:3, 4

g Kut 26:29

h Kut 26:1
1Fa 6:29i Kut 26:33
1Fa 8:6
Ebr 9:24

j 1Fa 6:20

k 1Fa 6:23-28

l 1Fa 8:6
1Nya 28:18

Safu ya 2

a Mt 27:51
Ebr 10:19, 20

b Kut 26:31, 33

c 2Fa 25:13

d 1Fa 7:15-22
2Fa 25:17
2Nya 4:11-13
Yer 52:22, 23

SURA YA 4

e Kut 38:1, 2
1Fa 8:22

no mitano nalo liligusa ukuta wa nyumba, na bawa la pili lilikuwa na urefu wa mikono mitano nalo liligusa bawa moja la kerubi wa pili. **12** Na bawa moja la kerubi wa pili lilikuwa na urefu wa mikono mitano nalo liligusa ukuta wa nyumba, na bawa la pili lilikuwa na urefu wa mikono mitano nalo liligusa bawa moja la yule kerubi wa kwanza. **13** Mabawa ya makerubi hao yalikuwa yamenyooshwa kufikia urefu wa mikono 20; nao walikuwa wamesimama kwa miguu yao, nyuso zao zikielekea ndani.*

14 Alitengeneza pia pazia^a kwa nyuzi za bluu, sufu ya zambarau, kitambaa chekundu, na kitambaa bora, na kulitarizi kwa mifano ya makerubi.^b

15 Kisha akatengeneza nguzo mbili^c mbele ya nyumba hiyo, zenye urefu wa mikono 35, na kifuniko kilichokuwa juu ya kila nguzo kilikuwa na urefu wa mikono mitano.^d

16 Pia alitengeneza minyororo iliyokuwa kama mikufu, akaiweka juu ya nguzo hizo, kisha akatengeneza makomamanga 100 na kuyaweka kwenye minyororo hiyo. **17** Akasimamisha nguzo hizo mbele ya hekalu, moja upande wa kulia* na nyingine upande wa kushoto;[#] akaiita nguzo ya upande wa kulia Yakini[^] na nguzo ya upande wa kushoto Boazi.[®]

4 Kisha akatengeneza madhabahu ya shaba^e yenye urefu wa mikono 20, upana wa mikono 20, na kimo cha mikono 10.

3:13 *Yaani, zikielekea Patakatifu. 3:17 *Au "kusini." #Au "kaskazini." ^Maana yake "Naye [yaani, Yehova] Aimarisha Kabisa." ®Labda inamaanisha "Katika Nguvu."

2 Alitengeneza Bahari*^a kwa madini yaliyoyeyushwa. Ilikuwa ya mvingo, yenye upana wa mikono 10 ukingo hadi ukingo na kimo cha mikono 5, na ingeweza kuzungukwa na kambe yenye urefu wa mikono 30.^b 3 Na chini yake kulikuwa na mapambo ya vibuyu,^c ambayo yalizunguka ukingo wote, vibuyu kumi kwa kila mkono mmoja kuzunguka Bahari yote. Vibuyu hivyo vilikuwa katika safu mbili, navyo vilitengenezwa kwa kuyeyushwa vikiwa sehemu ya Bahari hiyo. 4 Ilikuwa juu ya ng'ombe dume 12,^d watatu walitazama kaskazini, watatu walitazama magharibi, watatu walitazama kusini, na watatu walitazama mashariki; na Bahari hiyo ilikuwa juu yao, na sehemu zao zote za nyuma zilielekea katikati. 5 Na unene wake ulikuwa upana wa kiganja kimoja;* na ukingo wake ulitengenezwa kama ukingo wa kikombe, kama ua la yungiyungi. Ingeweza kujaa maji kiasi cha bathi 3,000.[#]

6 Pia, alitengeneza mabeseni kumi ya kuoshea, akaweka matano upande wa kulia na matano upande wa kushoto.^e Waliyatumia kuoshea vitu vilivyotumiwa kwa ajili ya dhahabu ya kuteketewa.^f Lakini Bahari ilitumiwa na makuhani kugea.^g

7 Kisha alitengeneza vinara kumi vya taa vya dhahabu,^h kulingana na maagizo,ⁱ akawitokea hekaluni, vitano upande wa kulia na vitano upande wa kushoto.^j

4:2 *Au "tangi." 4:5 *Karibu sentimita 7.4 (inchi 2.9). Angalia Nyongeza B14. #Bathi ilikuwa sawa na lita 22. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 4

a Kut 30:20
Kut 38:8

b 1Fa 7:23-26

c 1Fa 6:18

d Yer 52:20

e 1Fa 7:38, 39

f Law 1:9
Law 9:14

g Kut 29:4

h Kut 37:17

i 1Nya 28:12, 15

j Kut 40:24

Safu ya 2

a 2Nya 4:19

b Kut 27:9
Law 6:16

c 1Fa 6:36

d 1Fa 7:12

e 1Fa 7:39

f Kut 27:3

g 1Fa 7:40-46

h 2Nya 3:17

i 1Fa 7:17

j 1Fa 7:20

k Yer 52:22

l 1Fa 7:27, 38

m 1Fa 7:23, 25

n Kut 38:3

o 2Nya 2:13, 14

8 Alitengeneza pia meza kumi na kuziweka hekaluni, tano upande wa kulia na tano upande wa kushoto;^a naye alitengeneza mabakuli 100 ya dhahabu.

9 Kisha akatengeneza ua^b wa makuhani^c na ule ua mkuu^d na milango ya ua huo, akaifunika milango hiyo kwa shaba. 10 Akaiweka ile Bahari upande wa kulia, kuelekea kusini mashariki.^e

11 Hiram alitengeneza pia ndoo za kuondolea majivu, pia sepetu, na mabakuli.^f

Basi Hiram akamaliza kazi yote aliyomfanyia Mfalme Sulemani kuhusiana na nyumba ya Mungu wa kweli;^g 12 zile nguzo mbili^h na vifuniko vyenye umbo la bakuli vilivyokuwa juu ya nguzo hizo; na nyavu mbiliⁱ za kufunika vifuniko hivyo viwili vyenye umbo la bakuli vilivyokuwa juu ya nguzo hizo; 13 yale makomamanga 400^j kwa ajili ya zile nyavu mbili, safu mbili za makomamanga kwa ajili ya kila wavu, ili kufunika vile vifuniko viwili vyenye umbo la bakuli vilivyokuwa juu ya zile nguzo;^k 14 yale magari* kumi na yale mabeseni kumi yaliyokuwa juu ya magari hayo;^l 15 ile Bahari na wale ng'ombe dume 12 waliokuwa chini yake;^m 16 na ndoo za kuondolea majivu, sepetu, nyuma,ⁿ na vyombo vingine vyote ambavyo Hiram-abivu^o alitengenezea Mfalme Sulemani kwa shaba iliyong'arishwa kwa ajili ya nyumba ya Yehova. 17 Mfalme alitengeneza katika kalibu za udongo wa mfinyanzi katika wilaya ya

4:14 *Au "mikokoteni kumi ya maji."
4:16 *Wingi wa kifaa kinachoitwa uma.

Yordani kwenye eneo lenye udongo mwingi wa mfinyanzi, kati ya Sukothi^a na Sarethani. **18** Sulemani alitengeneza vyombo hivyo vyote kwa wingi sana; uzito wa shaba haukujulikana.^b

19 Sulemani alivitengeneza vitu vyote^c vya nyumba ya Mungu wa kweli: madhabahu ya dhahabu;^d meza^e na mikate ya wonyesho iliyokuwa juu ya meza hizo;^f **20** vinara vya taa na taa zake za dhahabu safi,^g ili ziwake mbele ya chumba cha ndani zaidi kulingana na maagizo; **21** na maua, taa, na koleo, vyote vya dhahabu, dhahabu safi kabisa; **22** mikasi ya kukatia tamba za taa, mabakuli, vikombe, na vyetezo, vyote vya dhahabu safi; na lango la nyumba, na milango ya ndani ya Patakatifu Zaidi,^h na milango ya nyumba ya hekalu, ya dhahabu.ⁱ

5 Kwa hiyo Sulemani akakamilisha kazi yote aliyopaswa kufanya kwa ajili ya nyumba ya Yehova. J Kisha Sulemani akaingiza ndani vitu ambavyo Daudi baba yake alikuwa amevifanya kuwa vitakatifu,^k naye akaweka fedha, dhahabu, na vitu vyote katika hazina za nyumba ya Mungu wa kweli.^l **2** Wakati huo Sulemani aliwakusanya wazee wa Israeli, viongozi wote wa makabila, wakuu wa koo* za Israeli. Wakaja Yerusalemu ili kuliondoa sanduku la agano la Yehova katika Jiji la Daudi,^m yaani, Sayuni.ⁿ **3** Wanaume wote wa Israeli walikusanyika mbele ya mfalme wakati wa sherehe* inayofanywa katika mwezi wa saba.^o

5:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.
5:3 *Yaani, Sherehe ya Vibanda.

SURA YA 4

a Yos 13:27, 28

b 1Fa 7:47
1Nya 22:3, 14
Yer 52:20

c 2Fa 24:13

d Kut 37:25, 26
Ufu 8:3e Kut 25:23, 24
2Nya 4:8

f 1Fa 7:48-50

g Kut 25:31, 37

h 1Fa 6:31, 32

i 1Fa 6:33-35

SURA YA 5

j 1Fa 6:38

k 1Nya 22:14

l 1Fa 7:51
1Nya 26:26m 2Sa 6:12
2Nya 1:4n 1Fa 8:1, 2
Zb 2:6o Law 23:34
2Nya 7:8

Safu ya 2

a Kut 25:14
Hes 4:15
1Fa 8:3-5
1Nya 15:2, 15b Kut 40:35
Hes 4:29, 31

c 2Sa 6:13

d 1Fa 6:20, 23
1Fa 8:6-9

e Kut 25:14

f Kut 34:1
Kut 40:20g Kut 19:5
Kut 24:7

h Kut 19:1

i Kut 19:10
Hes 8:21

j 1Nya 24:1

k 1Nya 15:16

l 1Nya 6:31, 39

m 1Nya 6:31, 33

n 1Nya 16:41
1Nya 25:1, 6
1Nya 25:3

4 Basi wazee wote wa Israeli wakaja, na Walawi wakalibeba Sanduku.^a **5** Wakalipandisha Sanduku, hema la mkutano,^b na vyombo vyote vitakatifu vilivyokuwa katika hema hilo. Makuhani na Walawi* wakavipandisha vitu hivyo. **6** Mfalme Sulemani na Waisraeli wote waliokusanywa ili waku-tane naye walikuwa mbele ya Sanduku. Kondoo na ng'ombe wengi sana wasiohesabika au kujulikana idadi walikuwa wakitolewa dhahabu.^c **7** Kisha makuhani wakalileta sanduku la agano la Yehova mahali pake, katika chumba cha ndani zaidi cha nyumba, yaani, Patakatifu Zaidi, chini ya mabawa ya makerubi.^d **8** Kwa hiyo mabawa ya makerubi yalikuwa yamenyoosha juu ya mahali ambapo Sanduku liliwekwa, hivi kwamba makerubi hao walilifunika Sanduku na fito zake.^e **9** Fito hizo zilikuwa ndefu sana hivi kwamba ncha zake zilionekana kutoka Patakatifu mbele ya chumba cha ndani zaidi, lakini hazikuonekana kutoka upande wa nje. Nazo ziko huko mpa-ka leo hii. **10** Hakukuwa na kitu kingine ndani ya Sanduku hilo isipokuwa yale mabamba mawili ambayo Musa aliyaweka humo kule Horebu,^f Yehova alipofanya agano^g na Waisraeli walipokuwa wakitoka Misri.^h **11** Makuhani walipotoka mahali patakatifu (kwa maana makuhani wote waliokuwepo walikuwa wamejitakasa,ⁱ bila kuzingatia vikundi vyao),^j **12** waimbaji wote Walawi^k walioongozwa na Asafu,^l Heman,^m Yeduthuni,ⁿ wana wao na ndugu zao walikuwa wa-

5:5 *Au "makuhani Walawi."

mevaa mavazi ya kitambaa bora, wakiwa wamebeba matoazi, vinanda, na vinubi; walikuwa wamesimama upande wa mashariki wa madhabahu, na makuhani 120 waliokuwa wakipiga tarumbeta walikuwa pamoja nao.^a **13** Mara tu wapiga tarumbeta na waimbaji walipoanza kumsifu na kumshukuru Yehova kwa pamoja, na milio ya tarumbeta, matoazi, na ala nyingine za muziki zilipoanza kusikika walipokuwa wakimsifu Yehova, “kwa maana yeye ni mwema; upendo wake mshikamainifu unadumu milele.”^b ndipo nyumba hiyo, nyumba ya Yehova, ikajaa wingu.^c **14** Makuhani hawakuweza kusimama ili kuhudumu kwa sababu ya wingu hilo, kwa maana utukufu wa Yehova ulijaa katika nyumba ya Mungu wa kweli.^d

6 Wakati huo Sulemani alisema: “Yehova alisema kwamba atakaa katika giza zito.^e **2** Sasa nimekujengea nyumba iliyokwezwa, mahali palipofanywa imara ili ukae humo milele.”^f

3 Kisha mfalme akageuka na kuanza kulibariki kutaniko lote la Waisraeli huku kutaniko lote la Waisraeli likiwa limesimama.^g **4** Akasema: “Na asifiwe Yehova Mungu wa Israeli, ambaye kwa kinywa chake mwenyewe alimwahidi baba yangu Daudi, na kwa mkono wake mwenyewe ametimiza, akisema, **5** ‘Kuanzia siku niliyowatoa watu wangu nchini Misri, sijachagua jiji katika makabila yote ya Israeli na kujenga humo nyumba ili jina langu likae humo,^h nami sijamchagua mwanamu me atakayekuwa kiongozi wa

SURA YA 5

a 1Nya 15:24

b 1Nya 16:34

c Kut 40:34, 35
1Fa 8:10, 11d 2Nya 7:1, 2
Eze 10:4
Ufu 21:23

SURA YA 6

e Kut 20:21
1Fa 8:12, 13
Zb 97:2

f Zb 132:13, 14

g 1Fa 8:14-21

h Kum 12:5, 6

Safu ya 2

a Zb 48:1

b 2Sa 7:8
1Nya 28:4c 2Sa 7:2
1Fa 5:3

d 1Nya 17:4

e 1Nya 28:5
1Nya 29:23

f 1Nya 17:11

g Kut 40:20
1Fa 8:9

h 1Fa 8:22

i 1Fa 6:36

watu wangu Waisraeli. **6** Lakini nimechagua Yerusalemu^a ili jina langu likae humo, nami nimechagua Daudi awatawale watu wangu Waisraeli.^b **7** Na moyo wa Daudi baba yangu ulitamani kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wa Israeli.^c **8** Lakini Yehova akamwambia Daudi baba yangu, ‘Moyo wako ulitamani kujenga nyumba kwa ajili ya jina langu, na ulifanya vizuri kutamani jambo hilo moyoni mwako. **9** Hata hivyo, hutajenga nyumba hiyo, lakini mwana wako mwenyewe utakayemzaa* ndiye atakayejenga nyumba hiyo kwa ajili ya jina langu.’^d **10** Yehova ametimiza ahadi hiyo aliyoitoa, kwa maana nimechukua mahali pa baba yangu Daudi na kuketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli,^e kama Yehova alivyoahidi.^f Pia nimejenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wa Israeli, **11** na humo nimeliweka Sanduku lenye agano^g ambalo Yehova alifanya na Waisraeli.”

12 Kisha akasimama mbele ya madhabahu ya Yehova mbele ya kutaniko lote la Waisraeli, akanyoosha mikono yake.^h **13** (Kwa maana Sulemani alikuwa amejennga jukwaa la shaba na kuliweka katikati ya ua.ⁱ Lili kuwa na urefu wa mikono mitano,* upana wa mikono mitano, na kimo cha mikono mitatu; akasimama juu yake.) Akapiga magoti mbele ya kutaniko lote la Waisraeli na kunyoosha mikono yake

6:9 *Tnn., “mwana wako, atakayetoka katika viuno vyako.” **6:13** *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

kuelekea mbinguni,^a **14** aka-sema: “Ee Yehova Mungu wa Israeli, hakuna Mungu kama wewe mbinguni wala duniani, unayeshika agano na kuwatendea kwa upendo mshikamanifu watumishi wako wanaotembea mbele zako kwa moyo wao wote.^b **15** Umetimiza ahadi uliyomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu.^c Ulitoa ahadi hiyo kwa kinywa chako mwenyewe, na siku ya leo umeitimiza kwa mkono wako mwenyewe.^d **16** Na sasa, Ee Yehova Mungu wa Israeli, timiza ahadi uliyomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu ulipomwambia, ‘Hutakosa kamwe mwanamume wa uzao wako atakayeketi kwenye kiti cha ufalme cha Israeli mbele zangu, ikiwa tu wana wako watakazia uangalifu njia yao kwa kutembea katika sheria yangu,^e kama ulivyotembea mbele zangu.^f **17** Na sasa, Ee Yehova Mungu wa Israeli, acha ahadi uliyomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu ithibitike kuwa ya kweli.

18 “Lakini Ee Mungu, je, kweli utakaa duniani pamoja na wanadamu?^g Tazama! Mbingu, naam, mbingu za mbingu, haziwezi kukutoshia,^h sembuse nyumba hii niliyoijenega!ⁱ **19** Sasa sikiliza sala yangu mimi mtumishi wako na ombi langu la kutaka kibali, Ee Yehova Mungu wangu, sikiliza kilio changu cha kuomba msaada na sala ambayo mimi mtumishi wako ninasali mbele zako. **20** Macho yako na yatazame nyumba hii usiku na mchana, yatazame mahali ambapo ulisema kwamba utaweka jina lako,^j ili usikilize

SURA YA 6

a 1Fa 8:54

b Kum 7:9
1Fa 8:23-26

c 1Fa 3:6

d 2Sa 7:12,13
1Nya 22:10

e Zb 132:12

f 1Fa 2:4

g Mdo 7:48

h 2Nya 2:6
Isa 40:12
Mdo 17:24i 1Fa 8:27-30
Isa 66:1

j Kum 26:2

Safu ya 2

a Da 6:10

b 2Fa 19:20
2Nya 30:27c 2Nya 7:12-14
Mik 7:18

d 1Fa 8:31, 32

e Ayu 34:11

f Isa 3:10, 11
Eze 18:20g Law 26:14, 17
Yos 7:8, 11
Amu 2:14

h Da 9:3, 19

i Ezr 9:5

j 1Fa 8:33, 34

k Isa 57:15

l Zb 106:47

m Law 26:19
Kum 28:23

sala ambayo mimi mtumishi wako ninasali kuelekea mahali hapa. **21** Nawe usikilize sihi zangu mimi mtumishi wako za kuomba msaada na sihi za watu wako Waisraeli wanaposali kuelekea mahali hapa,^a nawe usikilize katika makao yako, kutoka mbinguni;^b naam, usikilize na kusa-mehe.^c

22 “Mwanadamu akimtendea dhambi mwanadamu mwenzake, naye aapishwe* na kuwekwa chini ya wajibu wa kiapo hicho,^d naye akiwa chini ya kiapo^e aje mbele ya madhabahu yako katika nyumba hii,^f **23** basi usikie kutoka mbinguni na kuchukua hatua na kuwahukumu watumishi wako kwa kumlipa mwovu na kumwadhibu kwa sababu na jambo alilotenda*^e na kumtangaza mwadilifu kuwa asiye na hatia^f na kumthawabisha kulingana na uadilifu wake mwenyewe.^f

24 “Na watu wako Waisraeli wakishindwa na maadui kwa sababu ya kuzidi kukutendea dhambi,^g nao warudi na kilitukuza jina lako^h na kusaliⁱ na kukusihi wapate kibali mbele zako katika nyumba hii,^j **25** basi usikie kutoka mbinguni^k na kuwasamehe watu wako Waisraeli dhambi yao na kuwarudisha katika nchi uliyowapa wao na mababu zao.^l

26 “Mbingu zikifungwa ku siwe na mvua^m kwa sababu wamezidi kukutendea

6:22 *Au “aliyetendewa dhambi aki-mweka chini ya laana.” Yaani, kiapo kinacholeta laana ikiwa mtu anaapa kwa uwongo au kukosa kutimiza kiapo hicho. *Tnn., “laana.” **6:23** *Tnn., “kuleta juu ya kichwa chake mwenyewe jambo alilotenda.” *Tnn., “kuwa mwadilifu.”

dhambi,^a nao wasali kuelekea mahali hapa na kulitukuza jina lako na kuacha dhambi yao kwa sababu umewanyenyekeza,^{*b} **27** basi usikie kutoka mbinguni na kuwasamehe watumishi wako dhambi yao, dhambi ya watu wako Waisraeli, kwa sababu utawafundisha njia nzuri wanayopaswa kutembea ndani yake;^c na ulete mvua^d katika nchi yako ambayo uliwapata watu wako kuwa urithi.

28 "Njaa kali ikitokea nchini,^e au ugonjwa hatari,^f upepo unaochoma, kuvu,^g makundi ya nzige, au parare* wanaokula sana^h au maadui wao wakiwazingira katika jiji lote nchini^{#i} au pigo au ugonjwa wa aina yoyote ukitokea,^j **29** sala yoyote,^k ombi lolote la kutaka kibali^l ambalo huenda likatolewa na mtu yeyote au na watu wako wote Waisraeli (kwa sababu kila mmoja anajua mateso yake mwenyewe na maumivu yake mwenyewe)^m wakinyoosha mikono yao kuelekea nyumba hii,ⁿ **30** basi usikie kutoka mbinguni, makao yako,^o nawe usamehe;^p na umthawabishe kila mmoja kulingana na njia zake zote, kwa sababu unajua moyo wake (ni wewe peke yako unayejua vizuri moyo wa mwanadamu),^q **31** ili wakuogope kwa kutembea katika njia zako sikuzote watakazoishi katika nchi uliyowapa mababu zetu.

32 "Pia mgeni ambaye si sehemu ya watu wako Waisraeli na ambaye anatoka katika nchi ya mbali kwa sababu ya jina lako kuu*^r na mkono

6:26 *Au "umewatesa." **6:28** *Au "panzi." [#]Tnn., "katika nchi ya malango yake." **6:32** *Au "sifa yako."

SURA YA 6

- a Eze 14:13
b 1Fa 8:35, 36
c Isa 30:20, 21
Isa 54:13
d 1Fa 18:1
e Ru 1:1
2Fa 6:25
f Law 26:14, 16
Kum 28:21, 22
g Amo 4:9
Hag 2:17
h Kum 28:38
Yoe 1:4
i 2Nya 12:2
2Nya 32:1
j 1Fa 8:37-40
k 2Nya 20:5, 6
l 2Nya 33:13
m Met 14:10
n Da 6:10
o Isa 63:15
p Zb 130:4
q 1Sa 16:7
1Nya 28:9
Yer 11:20
Yer 17:10
r Kut 12:48
Ru 1:16
2Fa 5:15
Isa 56:6, 7
Mdo 8:27

Safu ya 2

- a 1Fa 8:41-43
b Zb 22:27
Zb 46:10
c Hes 31:2
Yos 8:1
Amu 1:1, 2
1Sa 15:3
d 2Nya 14:11
2Nya 20:5, 6
e 1Fa 8:44, 45
f Isa 37:36
g Zb 130:3
Mhu 7:20
Ro 3:23
h Law 26:34
1Fa 8:46-50
Da 9:7
i Law 26:40
Ezr 9:6
Ne 1:6
Zb 106:6
Da 9:5
j 1Sa 7:3
k Kum 30:1-3
Da 9:2, 3
l Da 6:10

wako wenye nguvu na mkono wako ulionyooosha, akija na kusali kuelekea nyumba hii,^a **33** basi usikilize kutoka mbinguni, makao yako, nawe ufanaye mambo yote ambayo mgeni huyo anakuomba ufanye, ili watu wote duniani wajue jina lako^b na kukuogopa, kama watu wako Waisraeli wanavyokuogopa, na ili wajue kwamba nyumba hii niliyojenga imeitwa kwa jina lako.

34 "Watu wako wakienda vitani kupigana na maadui wao mahali utakapowaelekeza^c nao wasali^d kwako kuelekea jiji hili ambalo umechagua na kuelekea nyumba ambayo nimejenga kwa ajili ya jina lako,^e **35** basi usikie kutoka mbinguni sala yao na ombi lao la kutaka kibali, nawe utekeleze hukumu kwa ajili yao.^f

36 "Wakikutendea dhambi (kwa sababu hakuna mwanadamu asiyetenda dhambi),^g nawe uwakasirikie vikali na kuwaacha mikononi mwa maadui, na waliowateka wawapeleke katika nchi fulani, mbali au karibu,^h **37** nao warudiwe na ufahamu wakiwa katika nchi ya watu waliowachukua mateka, na kukurudia na kukuomba kibali katika nchi walikopelekwa mateka, wakisema, "Tumetenda dhambi na kukosea; tumetenda uovu,"ⁱ **38** nao wakurudie kwa moyo wao wote^j na kwa nafsi* yao yote katika nchi walikopelekwa mateka,^k nao wasali kwako kuelekea nchi yao ambayo uliwapata mababu zao na kuelekea jiji ambalo umelichagua^l na nyumba ambayo nimejenga kwa ajili ya jina lako, **39** basi usikie

6:38 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

kutoka mbinguni, makao yako, sala yao na ombi lao la kutaka kibali, nawe utekeleze hukumu kwa ajili yao^a na uwasamehe watu wako ambao wamekutendea dhabihu.

40 “Sasa, Ee Mungu wangu, tafadhali, macho yako yatazame na masikio yako yasililize kwa makini sala inayotolewa* mahali hapa.^b **41** Na sasa, Ee Yehova Mungu, pandu uingie mahali pako pa kumpuzikia,^c wewe pamoja na Sanduku la nguvu zako. Makuhani wako, Ee Yehova Mungu, na wavishwe wokuvu, na acha washikamanifu wako washangilie kwa sababu ya wema wako.^d **42** Ee Yehova Mungu, usimkatae* mtiwamafuta wako.^e Ukumbuke upendo wako mshikamanifu kwa Daudi mtumishi wako.”^f

7 Basi, mara tu Sulemani alipomaliza kusali,^g moto ulishuka kutoka mbinguni^h ukateketeza ile dhabihu ya kuteketezwa na dhabihu nyinginezo, na utukufu wa Yehova ukajaa katika nyumba hiyo.ⁱ **2** Makuhani hawakuweza kuingia ndani ya nyumba ya Yehova kwa sababu utukufu wa Yehova ulikuwa umejaa katika nyumba ya Yehova.^j **3** Waisraeli wote walikuwa wakitazama moto uliposhuka na utukufu wa Yehova ulipokuwa juu ya nyumba hiyo, nao wakainama kifudifudi kwenye sakafu ya mawe, wakasujudu na kumshukuru Yehova, “kwa maana yeye ni mwema; upendo wake mshikamanifu unadumu milele.”

4 Sasa mfalme na watu

6:40 *Au “inayohusu.” **6:42** *Tnn., “usiugeuzie mbali uso wa.”

SURA YA 6

a Yer 51:36, 37

b 2Nya 7:15
2Nya 16:9
Zb 65:2
Isa 37:17

c 1Nya 28:2

d Zb 65:4
Zb 132:8-10

e 1Fa 1:34
Zb 18:50

f Mdo 13:34

SURA YA 7

g 1Fa 8:54

h Law 9:24
1Nya 21:26

i Kut 40:34, 35

j 1Fa 8:11

Safu ya 2

a 1Fa 8:62, 63

b Ezr 6:16

c 1Nya 25:7
2Nya 5:11, 12

d 2Nya 5:13

e Law 1:3

f 2Nya 4:1

g Law 2:1

h Law 4:8-10
1Fa 8:64-66

i Law 23:34
Kum 16:13

j Hes 34:2, 5, 8

k Law 23:36

wote wakazitoa dhabihu mbele za Yehova.^a **5** Mfalme Sulemani alitoa ng'ombe 22,000 na kondoo 120,000 kuwa dhabihu. Basi mfalme na watu wote wakaizindua nyumba ya Mungu wa kweli.^b **6** Makuhani walikuwa wamesimama katika vituo vyao vya kazi, na Walawi pia waliokuwa na ala za muziki zilizopigwa kuambata na nyimbo ambazo Yehova aliimbiwa.^c (Mfalme Daudi alikuwa ametengeneza ala hizo ili kumshukuru Yehova —“kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele”—wakati Daudi alipokuwa akitoa sifa pamoja nao.*) Na makuhani walikuwa wakipiga tarumbeta kwa sauti kubwa^d mbele yao, huku Waisraeli wote wakiwa wamesimama.

7 Kisha Sulemani akataka-sehemu ya katikati ya ua uliokuwa mbele ya nyumba ya Yehova, kwa maana alipaswa kutolea mahali hapo dhabihu za kuteketezwa^e na vipande vya mafuta vya dhabihu za ushirika, kwa sababu madhabahu ya shaba^f ambayo Sulemani alikuwa amejenga haingeweza kutoshea dhabihu za kuteketezwa, matoleo ya nafaka,^g na vipande vya mafuta.^h **8** Wakati huo Sulemani alifanya sherehe hiyo kwa siku sabaⁱ pamoja na Waisraeli wote, kutaniko kubwa sana kuanzia Lebo-hamathi* kushuka mpaka kwenye Korongo[#] la Misri.^j **9** Lakini siku ya nane* walifanya kusanyiko takatifu,^k kwa sababu wali-

7:6 *Huenda ni Walawi. **7:8** *Au “njia ya kuingia Hamathi.” [#]Angalia Kamusi, uku. 2012. **7:9** *Siku ya kwanza baada ya sherehe hiyo, au siku ya 15.

kuwa wameizindua madhabahu kwa siku saba na kufanya sherehe hiyo kwa siku saba. **10** Kisha siku ya 23 ya mwezi wa saba, aliwaruhusu watu waende nyumbani kwao wakishangilia^a na kufurahi moyoni kwa sababu ya wema ambao Yehova alikuwa amemtendea Daudi na Sulemani na watu wake Waisraeli.^b

11 Kwa hiyo Sulemani akakamilisha nyumba ya Yehova na nyumba ya* mfalme;^c na kila kitu ambacho Sulemani alitamani moyoni mwake kufanya kuhusiana na nyumba ya Yehova na nyumba yake mwenyewe, alifanikiwa kukitimizia.^d **12** Kisha Yehova akamotokea Sulemani^e usiku na kumwambia: “Nimesikia sala yako, nami nimechagua mahali hapa kwa ajili yangu ili pawe nyumba ya dhabihu.^f **13** Nikifunga mbingu ili mvua isinyeshe, nami nikiamuru panzi waile nchi, nami nikilita ugonjwa hatari miongoni mwa watu wangu, **14** na watu wangu ambao wameitwa kwa jina langu^g wakijinyenyekeza^h na kusali na kuutafuta uso wangu na kuacha njia zao ovu,ⁱ ndipo nitakaposikia kutoka mbinguni na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao.^j **15** Sasa macho yangu yatatazama na masikio yangu yatasikiliza kwa makini sala zinazotolewa mahali hapa.^k **16** Na sasa nimeichagua nyumba hii na kuitakasa ili jina langu likae humu milele,^l na macho yangu na moyo wangu utakuwa humu siku zote.^m

17 “Nawe, ukitembea mbele

7:11 *Au “jumba la.”

SURA YA 7

- a Kum 16:15
b 2Nya 6:41
c Mhu 2:4
d 1Fa 9:1-3
e 2Nya 1:7
f Kum 12:5, 6
Zb 78:68
g Isa 43:10
h Law 26:41
2Nya 33:12, 13
i Isa 55:7
j 2Nya 6:39
k 2Nya 6:40
l Kum 12:21
m 2Nya 6:20

Safu ya 2

- a 1Fa 9:4, 5
b 2Sa 7:12, 13
c Zb 89:28, 29
d 1Fa 2:4
e Kut 20:5
1Fa 9:6-9
f Kum 4:25, 26
2Fa 17:20
g Kum 28:37
Yer 24:9
h 2Nya 29:8
Da 9:12
i Kum 29:24, 25
2Fa 25:8, 9
Yer 22:8, 9
j 2Nya 15:2
k Kut 12:51
l Isa 2:8
Yer 2:11
m 2Nya 36:17

SURA YA 8

- n 1Fa 6:37, 38
1Fa 7:1
1Fa 9:10
o 1Fa 5:1

2 MAMBO YA NYAKATI 7:10-8:2

zangu kama Daudi baba yako alivyotembea, kwa kutenda mambo yote niliyokuamuru, nawe ukitii masharti yangu na sheria* zangu,^a **18** ndipo nitakapoirarisha kiti cha ufalme wako,^b kama nilivyofanya agano pamoja na Daudi baba yako,^c niliposema, ‘Hutakosa kamwe mwanamume wa uzao wako atakayetawala Israeli.’^d **19** Lakini ikiwa utageuka na kuacha maagizo yangu na amri zangu ambazo nimeweka mbele yako, nawe uende na kuabudu miungu mingine na kuiinamia,^e **20** nitawang’oa Waisraeli kutoka katika nchi ambayo nimewapa,^f na nyumba hii ambayo nimeitakasa kwa ajili ya jina langu nitaitupilia mbali kutoka mbele za macho yangu, nami nitaifanya iwe kitu cha kudharauliwa* na kitu cha kudhihakiwa miongoni mwa mataifa yote.^g **21** Na nyumba hii itakuwa marundo ya magofu. Kila mtu atakayepita karibu nayo ataitazama kwa mshangao^h na kuuliza, ‘Kwa nini Yehova aliitendea hivi nchi hii na nyumba hii?’ⁱ **22** Kisha watasema, ‘Ni kwa sababu walimwacha Yehova/ Mungu wa mababu zao, aliye watoa nchini Misri,^k nao wakashikamana na miungu mingine, wakaiinamia na kuiabudu.^l Ndiyo sababu aliwaletea msiba huo wote.’^m

8 Katika muda wa miaka 20 ambayo Sulemani alijenga nyumba ya Yehova na nyumba yake* mwenyewe,ⁿ **2** Sulemani alijenga upya majiji ambayo Hiram^o alikuwa amepa, akawapa Waisraeli*

7:17 *Tnn., “hukumu.” 7:20 *Tnn., “methali.” 8:1 *Au “jumba lake.” 8:2 *Tnn., “wana wa Israeli.”

waishi humo. **3** Isitoshe, Sulemani alienda Hamath-soba na kuliteka jiji hilo. **4** Kisha akajenga tena jiji la Tadmori kule nyikani na majiji yote yenye maghala^a aliyokuwa amejenga Hamathi.^b **5** Alijenga pia Beth-horoni ya Juu^c na Beth-horoni ya Chini,^d majiji yenye ngome yaliyokuwa na kuta, malango, na makomeo, **6** na Baalathi^e na pia majiji yote ya Sulemani yenye maghala, majiji yote ya magari ya vita,^f majiji ya wapanda farasi, na chochote ambacho Sulemani alitamani kujenga huko Yerusalemu, Lebanoni, na katika nchi yote iliyokuwa chini ya mamlaka yake.

7 Na watu wote waliobaki, yaani, Wahiti, Waamori, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi^g ambao hawakuwa sehemu ya Waisraeli,^h **8** wazao wao waliobaki nchini—wale ambao Waisraeli hawakuwaangamizaⁱ—Sulemani aliwaandikisha ili wafanye kazi ya kulazimishwa mpaka leo hii.^j **9** Lakini Sulemani hakumfanya Mwisraeli yeyote kuwa mtumwa wake,^k kwa sababu walikuwa mashujaa wake, wakuu wa makamanda wake wasaidizi, na wakuu wa waendeshaji wa magari yake ya vita na wapanda farasi wake.^l **10** Kulikuwa na wakuu 250 wa wasaidizi wa Mfalme Sulemani, walio-kuwa wasimamizi wa watu.^m

11 Pia, Sulemani alimtoa binti ya Faraoⁿ kutoka katika Jiji la Daudi na kumpeleka katika nyumba aliyokuwa amejengea,^o kwa maana alisema: “Ingawa ni mke wangu, hapaswi kukaa katika nyumba ya Mfalme Daudi wa Israeli, kwa sababu sehemu ambazo Sa-

SURA YA 8

a 1Fa 9:17-19

b 2Fa 14:28

c Yos 16:5

d Yos 16:1, 3
1Nya 7:24

e Yos 19:44, 48

f 1Fa 4:26

g Mwa 15:18-21
Hes 13:29

h 1Fa 9:20-23

i Yos 15:63
Yos 17:12j Yos 16:10
2Nya 2:17, 18

k Law 25:39

l 1Sa 8:11, 12

m 1Fa 5:16
1Fa 9:23
2Nya 2:18

n 1Fa 3:1

o 1Fa 7:8
1Fa 9:24

Safu ya 2

a Kut 29:43

b Law 1:3

c 2Nya 4:1

d 1Fa 6:3

e Hes 28:9

f Hes 28:11-15

g Kum 16:16

h Law 23:6

i Law 23:15, 16

j Law 23:34

k 1Nya 24:1

l 1Nya 6:31, 32
1Nya 15:16
1Nya 16:37, 42
1Nya 25:1

m 1Nya 26:1

n 1Fa 6:1

o 1Fa 7:51

p Hes 33:1, 35
1Fa 22:48q Kum 2:8
2Fa 14:21, 22
2Fa 16:6

r 1Fa 9:26-28

s 2Sa 5:11

nduku la Yehova limeletwa ni takatifu.”^a

12 Kisha Sulemani akamtolea Yehova dhabihu za kuteketezwa^b kwenye madhabahu^c ya Yehova aliyokuwa amejenga mbele ya ukumbi.^d

13 Alifuata utaratibu wa kila siku kwa kutoa dhabihu kulingana na amri ya Musa iliyo-husu Sabato,^e miezi mipya,^f na sherehe zilizoamriwa mara tatu kwa mwaka^g—Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu,^h Sherehe ya Majuma,ⁱ na Sherehe ya Vibanda.^{*j} **14** Pia, alipanga vikundi vya makuhani^k kwa ajili ya utumishi wao kulingana na sheria ya Daudi baba yake, na Walawi katika vituo vyao vya kazi, ili watoe sifa^l na kuhudumu mbele ya makuhani kulingana na utaratibu wa kila siku, na walinzi wa malango katika vikundi vyao kwenye malango mbalimbali,^m kwa maana hivyo ndivyo alivyoamuru Daudi, mtu wa Mungu wa kweli. **15** Nao hawakuacha amri ambayo mfalme aliwapa makuhani na Walawi kuhusiana na jambo lolote au kuhusiana na maghala. **16** Basi kazi yote ya Sulemani ilipangwa vizuri sana,^{*} kuanzia siku ambayo msingi wa nyumba ya Yehova uliwekwaⁿ mpaka ilipomalizwa. Basi nyumba ya Yehova ikakamilishwa.^o

17 Huo ndio wakati ambapo Sulemani alienda Esiongeberi^p na Elothi^q kwenye ufuo wa bahari katika nchi ya Edomu.^r **18** Hiram^s aliwatumia watumishi wake mwenyewe wampelekee meli na ma-

8:13 *Au “Vibanda vya Muda.” **8:16** *Au “Ilikuwa na mpangilio mzuri; ilikamilishwa.”

baharia wenye uzoefu. Wakenda Ofiri^a pamoja na watumishi wa Sulemani, wakachukua huko talanta 450* za dhahabu^b na kumletea Mfalme Sulemani.^c

9 Basi malkia wa Sheba^d alisikia habari za Sulemani, kwa hiyo akaja Yerusalemu kumjaribu kwa maswali magumu.* Alikuwa na msafara wenye kuvutia sana, pamoja na ngamia waliobeba mafuta ya zeri na dhahabu nyingi sana^e na mawe yenye thamani. Akafika mbele ya Sulemani na kumwambia mambo yote yaliyokuwa moyoni mwake.^f **2** Kisha Sulemani akajibu maswali yake yote. Hakuna jambo lolote lililokuwa gumu sana* kwa Sulemani asiweze kumweleza.

3 Malkia wa Sheba alipoo-na hekima yote ya Sulemani,^g nyumba aliyojenga,^h **4** chakula kilichokuwa meza-ni pake,ⁱ jinsi watumishi wake walivyoketi, jinsi watumishi wake walivyohudumu mezani na pia mavazi yao, na wale waliompa vinywaji na jinsi walivyovalia, na dhabihu zake za kutekelezwa alizotoa kwa ukawaida katika nyumba ya Yehova,^j alipigwa na bumbuazi.* **5** Basi akamwambia mfalme: "Habari nilizosikia katika nchi yangu kuhusu mafanikio* yako na kuhusu hekima yako zilikuwa za kweli. **6** Lakini sikuamini habari hizo mpaka nilipokuja na kujionea kwa macho yangu mwenyewe.^k Na kwa kweli si-

8:18; 9:9 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. **9:1** *Au "mafumbo." **9:2** *Tnn., "lililofichwa." **9:4** *Tnn., "hakubaki na roho yoyote ndani yake." **9:5** *Au "m-
neno."

SURA YA 8

a 1Fa 22:48
Zb 45:9

b 1Fa 10:22

c Mhu 2:8

SURA YA 9

d Mt 12:42
Lu 11:31

e Zb 72:15

f 1Fa 10:1-3

g 1Fa 3:28
Mhu 12:9

h 1Fa 10:4-9

i 1Fa 4:22, 23

j 2Nya 8:12, 13

k Lu 11:31

Safu ya 2

a Mhu 1:16

b 1Fa 4:31, 34
2Nya 1:11, 12

c 2Nya 2:11

d Zb 72:10

e 1Fa 10:10

f 1Fa 9:27, 28
1Fa 10:22
2Nya 8:18

g 1Fa 10:11, 12

h 1Fa 6:8

i 1Fa 7:1

j 1Nya 25:1
Zb 92:3

kuwa nimeambiwa hata nusu ya hekima yako nyingi.^a Umezidi kwa mbali habari nilizosikia.^b **7** Wenye furaha ni watu wako, na wenye furaha ni watumishi wako wanaosimama mbele yako daima, wakiisikiliza hekima yako! **8** Na asifiwe Yehova Mungu wako, ambaye amependezwa nawe, akakuweka kwenye kiti chake cha ufalme ukiwa mfalme kwa niaba ya Yehova Mungu wako. Kwa sababu Mungu wako anawapenda Waisraeli,^c na ili kuwafanya wadumu milele, alikuweka kuwa mfalme juu yao ili utekeleze haki na uadilifu."

9 Kisha akampa mfalme talanta 120* za dhahabu^d na kiasi kikubwa sana cha mafuta ya zeri na mawe yenye thamani. Mfalme Sulemani hakuwahi tena kuletewa kiasi kikubwa hivyo cha mafuta ya zeri kama alichotetewa na malkia wa Sheba.^e

10 Isitoshe, watumishi wa Hiram na watumishi wa Sulemani ambao walileta dhahabu kutoka Ofiri,^f walileta pia mbao za misandali na mawe yenye thamani.^g **11** Mfalme alitumia mbao hizo za misandali kutengeneza ngazi za nyumba ya Yehova,^h na nyumba ya* mfalme,ⁱ na pia vinubi na vinanda vya waimbaji.^j Mbao kama hizo hazikuwa zimewahi kuonekana katika nchi ya Yuda.

12 Mfalme Sulemani alimpa pia malkia wa Sheba kitu chochote alichotamani na kuomba, zaidi ya* vitu alivyomletea mfalme. Kisha

9:11 *Au "jumba la." **9:12** *Au labda, "pamoja na zawadi zilizolingana na thamani ya."

akaondoka na kurudi katika nchi yake, pamoja na watumishi wake.^a

13 Na dhahabu iliyoletwa kwa Sulemani katika mwaka mmoja ilikuwa na uzito wa talanta 666 za dhahabu,^b

14 mbali na dhahabu iliyole-twa na wafanyabiashara wasa-firi na wauzaji wa bidhaa na wafalme wote wa Uarabuni na magavana wa nchi walioku-wa wakimletea Sulemani dhahabu na fedha.^c

15 Mfalme Sulemani alite-ngeneza ngao kubwa 200 za dhahabu iliyochanganywa na madini mengine^d (kwa kila ngao alitumia shekeli 600* za dhahabu hiyo)^e **16** na ngao ndogo* 300 za dhahabu iliyo-changanywa na madini mengi-ne (kwa kila ngao ndogo alitumia mina tatu^f za dhahabu). Kisha mfalme akaziweka katika Nyumba ya Msitu wa Lebanoni.^f

17 Mfalme pia alitengeneza kiti kikubwa cha ufalme cha pembe za tembo na kukifunika kwa dhahabu safi.^g

18 Kiti hicho cha ufalme kilikuwa na ngazi sita, nacho kiliunganishwa na kiti cha miguu cha dhahabu, na kilikuwa pia na mikono pande zote mbili, na simba wawili^h walisimama kando ya mikono hiyo. **19** Na kulikuwa na simba 12ⁱ waliosimama kwenye ngazi hizo sita, wawili kwenye kila ngazi, mmoja upande huu na mwingine upande wa pili. Hakuna ufalme

9:15 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. 9:16 *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale. ^fKatika Maandiko ya Kiebrania mina moja inalingana na gramu 570. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 9

a 1Fa 10:13

b 1Fa 10:14, 15
2Nya 1:15
Zb 68:29
Zb 72:15

c Zb 72:10

d 2Nya 12:9

e 1Fa 10:16, 17

f 1Fa 7:2

g 1Fa 10:18-20

h Mwa 49:9

i Hes 23:24

Safu ya 2

a 1Fa 10:21, 22
1Fa 10:27b Zb 72:10
Yon 1:3

c 1Fa 9:27

d 1Fa 10:18

e 1Fa 3:12, 13
1Fa 4:29
1Fa 10:23-25f 1Fa 3:28
1Fa 4:34
2Nya 1:12
Met 2:6

g Mt 6:29

h Kum 17:16
1Fa 4:26

i 1Fa 10:26

j 1Fa 4:21

mwingine wowote uliokuwa umetengeneza kiti kama hicho. **20** Vyombo vyote vya kunywea vya Mfalme Sulemani vilikuwa vya dhahabu, na vyombo vyote vya Nyumba ya Msitu wa Lebanoni vilikuwa vya dhahabu safi. Hakukuwa na kiti chochote kilichotengenezwa kwa fedha, kwa maana fedha ilionwa kuwa si kiti katika siku za Sulemani.^a

21 Kwa maana meli za mfalme zilikuwa zikienda Tarshishi^b na watumishi wa Hiram.^c Mara moja baada ya kila miaka mitatu, meli za Tarshishi zilikuja zikiwa zimejazwa dhahabu na fedha, pembe za tembo,^d sokwe, na tausi.

22 Kwa hiyo Mfalme Sulemani alikuwa na utajiri mwingi zaidi na hekima kuliko wafalme wengine wote duniani.^e

23 Na wafalme wote duniani walitaka kukutana na* Sulemani ili wasikie hekima yake ambayo Mungu wa kweli alikuwa ameweka moyoni mwake.^f **24** Kila mmoja wao alileta zawadi—vitu vya fedha, vitu vya dhahabu, mavazi,^g silaha, mafuta ya zeri, farasi, na nyumbu—na walifanya hivyo mwaka baada ya mwaka.

25 Na Sulemani alikuwa na mabanda 4,000 kwa ajili ya farasi wake na magari yake ya vita na pia alikuwa na farasi* 12,000,^h naye aliwaweka katika majiji ya magari ya vita karibu naye huko Yerusalemu.ⁱ **26** Naye aliwatawala wafalme wote kuanzia Mto Efrati mpaka nchi ya Wafilisti hadi kwenye mpaka wa Misri.^j **27** Mfalme alifanya fedha huko Yerusalemu iwe nyingi

9:23 *Tnn., "waliutafuta uso wa." 9:25 *Au "wapanda farasi."

kama mawe, na mbao za mie-rezi ziwe nyingi kama mikuyu katika Shefela.^a **28** Nao walikuwa wakimlelea Sulemani farasi kutoka Misri^b na kutoka katika nchi nyingine zote.

29 Na mambo mengine katika historia ya Sulemani,^c kuanzia mwanzo mpaka mwisho, je, hayajaandikwa katika maandishi ya nabii Nathani,^d katika unabii wa Ahiya^e Mshilo, na katika kumbukumbu ya maono ya mwonaji Ido^f kumhusu Yeroboamu^g mwana wa Nebati? **30** Sulemani alitawala nchi yote ya Israeli kwa miaka 40 akiwa Yerusalemu. **31** Kisha Sulemani akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake. Basi wakamzika katika Jiji la Daudi baba yake;^h na Rehoboamu mwanawe akawa mfalme baada yake.ⁱ

10 Rehoboamu alienda Shekemu,^j kwa maana Waisraeli wote walikuwa wamekuja Shekemu kumfanya kuwa mfalme.^k **2** Mara tu Yeroboamu^l mwana wa Nebati aliposikia habari hizo (bado alikuwa akiishi Misri kwa saba alikuwa amemkimbia Mfalme Sulemani),^m akarudi kutoka Misri. **3** Ndipo wakatuma watu waende kumwita, kisha Yeroboamu na Waisraeli wote wakaja kwa Rehoboamu na kumwambia hivi: **4** “Baba yako aliifanya nira yetu kuwa nzito.ⁿ Lakini ukiufanya utumishi mzito wa baba yako kuwa mwepesi zaidi na kupunguza nira nzito* aliyo-tutwika, tutakutumikia.”

5 Ndipo akawaambia: “Rudini kwangu baada ya siku tatu.” Basi watu wakaenda

10:4 *Au “inayokandamiza.”

SURA YA 9

a 1Fa 10:27
1Nya 27:28

b 1Fa 10:28
2Nya 1:16

c 1Fa 11:41-43

d 2Sa 7:2
2Sa 12:1
1Fa 1:8
1Nya 29:29

e 1Fa 11:30, 31
1Fa 14:2
1Fa 14:6, 10

f 2Nya 12:15
2Nya 13:22

g 1Fa 11:26

h 2Sa 5:9
1Fa 2:10

i 1Fa 14:21

SURA YA 10

j Yos 20:7
Yos 24:1
Amu 9:1

k 1Fa 12:1-4

l 1Fa 11:28

m 1Fa 11:40

n 1Sa 8:11-18
1Fa 4:7

Safu ya 2

a 1Fa 12:5-7

b 1Fa 12:8-11

c 1Fa 12:12-15

zao.^a **6** Kisha Mfalme Rehoboamu akashauriana na wanaume wazee waliomtumikia Sulemani baba yake alipokuwa hai, akawauliza: “Mnani-shauri niwape jibu gani watu hawa?” **7** Wakamjibu: “Ukiwa mwema kwa watu hawa na kuwafurahisha na kuwapa jibu linalofaa, watakuwa watumishi wako sikuzote.”

8 Hata hivyo, alikataa ushauri aliopeva na wanaume wazee, akashauriana na vijana wa rika lake na ambao sasa walikuwa watumishi wake.^b

9 Aliwauliza: “Mnashauri tuwape jibu gani watu hawa ambao wameniambia, ‘Ifanye nira ambayo baba yako alitutwika iwe nyepesi zaidi?’” **10** Vijana hao wa rika lake wakamwambia: “Hivi ndivyo unavyopaswa kuwaambia watu waliokwambia, ‘Baba yako aliifanya nira yetu kuwa nzito, lakini wewe unapaswa kuifanya kuwa nyepesi zaidi kwa ajili yetu’; hivi ndivyo unavyopaswa kuwaambia, ‘Kidole changu kidogo kitakuwa kinene kuliko kiuno cha baba yangu. **11** Baba yangu aliwatwika nira nzito, lakini mimi nitazidisha uzito wa nira yenu. Baba yangu aliwaadhibu kwa mijeledi, lakini mimi nitawaadhibu kwa mijeledi yenye miiba.”

12 Yeroboamu na watu wote wakaja kwa Rehoboamu siku ya tatu, kama mfalme alivyokuwa amesema: “Rudini kwangu siku ya tatu.”^c

13 Lakini mfalme akawajibu kwa ukali. Kwa hiyo Mfalme Rehoboamu akakataa ushauri wa wanaume wazee. **14** Akawajibu kama alivyoshauriwa na vijana wa rika lake, na

kusema: “Nitafanya nira yenu iwe nzito zaidi, nami nita-zidisha uzito wake. Baba ya-angu aliwaadhibu kwa mijeledi, lakini mimi nitawaadhibu kwa mijeledi yenye miiba.” **15** Basi mfalme hakuwasikiliza watu, kwa sababu Mungu wa kweli ndiye aliyesababisha badiliko hilo la mambo,^a ili atimize neno ambalo Yehova alimwambia Yeroboamu mwana wa Nebati kupitia Ahiya Mshilo.^b

16 Waisraeli wote walipoo-na kwamba mfalme amekataa kuwasikiliza, wakamwambia hivi mfalme: “Tuna ushirikagani na Daudi? Hatuna urithi wowote katika mwana wa Yese. Kila mtu aende kwa miungu yake, enyi Waisraeli! Sasa itunze nyumba yako mwenyewe, Ee Daudi.”^c Ndipo Waisraeli wote wakarudi katika nyumba zao.^{*d}

17 Lakini Rehoboamu akae-ndelea kuwatawala Waisraeli walioishi katika majiji ya Yuda.^e

18 Kisha Mfalme Rehoboamu akamtuma Hadoramu,^f aliyekuwa msimamizi wa watu waliofanya kazi ya kulazimishwa, lakini Waisraeli wote wakamuua kwa kumpiga mawe. Mfalme Rehoboamu akafaulu kupanda gari lake na kukimbilia Yerusalemu.^g **19** Na tangu siku hiyo Waisraeli wamekuwa wakiasi nyumba ya Daudi.

11 Rehoboamu alipofika Yerusalemu, mara moja aliikusanya nyumba ya Yuda na kabila la Benjamini,^h mashujaa 180,000 waliozoezwa,^{*}

10:16 *Tnn., “mahema yao.” 11:1 *Tnn., “waliochaguliwa.”

SURA YA 10

a Kum 2:30
2Sa 17:14

b 1Fa 11:29-31

c 1Fa 11:32

d 1Fa 12:16,17

e 1Fa 11:35, 36

f 2Sa 20:24
1Fa 4:6

g 1Fa 12:18, 19

SURA YA 11

h Mwa 49:27
2Nya 14:8

Safu ya 2

a 1Fa 12:21-24

b 2Nya 12:15

c 1Fa 11:31
2Nya 10:15

d Mwa 35:19
Mt 2:1

e Amo 1:1

f 2Nya 28:18

g 1Sa 22:1

h 1Nya 18:1

i 1Sa 23:14

j 2Nya 32:9

k Yos 10:10
Yer 34:7

l Yos 19:42, 48

m Yos 14:14, 15
2Sa 2:1

n Hes 35:2, 3

ili wapigane na Waisraeli na kuurudisha ufalme kwa Rehoboamu.^a **2** Kisha neno hili la Yehova likamjia Shema-ya^b mtu wa Mungu wa kweli: **3** “Mwambie Rehoboamu mwana wa Sulemani mfalme wa Yuda na Waisraeli wote walio Yuda na Benjamini, **4** ‘Hivi ndivyo Yehova anavyosema: “Msipande kwen-nda kupigana na ndugu zenu. Kila mmoja wenu arudi nyumbani kwake, kwa maana nimesababisha mambo haya yatu-kie.””^c Basi wakalitii neno la Yehova na kurudi, nao hawakwenda kupigana na Yeroboamu.

5 Rehoboamu aliishi Yerusalemu na kujenga majiji yenye ngome huko Yuda. **6** Basi akajenga^{*} Bethlehemi,^d Etamu, Tekoa,^e **7** Beth-suri, Soko,^f Adulamu,^g **8** Gathi,^h Maresha, Zifu,ⁱ **9** Adoraimu, Lakishi,^j Azeka,^k **10** Sora, Aiyaloni,^l na Hebroni,^m majiji yenye ngome yaliyokuwa Yuda na Benjamini. **11** Pia, alii-marisha maeneo yenye ngome, akawaweka makamanda humo na kuwapa chakula na mafuta na divai, **12** naye akapeleka ngao kubwa na mikuki katika majiji yote mbalimbali; akayamarisha kwa kiwango kikubwa sana. Na majiji ya Yuda na Benjamini ya-kaendelea kuwa yake.

13 Na makuhani na Walawi waliokuwa katika nchi yote ya Israeli wakamuunga mko-no, wakaja kutoka katika maeneo yao yote. **14** Walawi waliacha malisho yao na miliki yaoⁿ wakaja Yuda na Yerusalemu, kwa sababu Yeroboamu

11:6 *Au “akaimarisha.”

na wanawe walikuwa wame-waondoa ili wasiwe makuhani wa Yehova.^a **15** Kisha Yero-boamu akawaweka makuhani wake mwenyewe ili wahu-dumu mahali pa juu^b na kuwatumikia roho waovu we-nyye umbo la mbuzi*^c na ndama aliokuwa ametengeneza.^d **16** Na watu kutoka katika makabila yote ya Israeli waliokuwa wameazimia moyoni mwao kumtafuta Yehova Mungu wa Israeli wakawafuata mpaka Yerusalemu ili kumtolea dhahibu Yehova Mungu wa mababu zao.^e **17** Kwa miaka mitatu waliuimarisha ufalme wa Yuda na kumuunga mkono Rehoboamu mwana wa Sulemani, kwa maana walitembea katika njia ya Daudi na Sulemani kwa miaka mitatu.

18 Kisha Rehoboamu akamwoa Mahalathi binti ya Yeri-mothi mwana wa Daudi na wa Abihaili binti ya Eliabu^f mwana wa Yese. **19** Baada ya muda akamzalia wana hawa: Yeushi, Shemaria, na Zahamu. **20** Kisha akamwoa Maaka mjukuu wa Absalomu.^g Baada ya muda akamzalia Abiya,^h Atai, Ziza, na Shelomithi. **21** Rehoboamu alimpenda zaidi Maaka mjukuu wa Absalomu kuliko wake zake wengine wote na masuriaⁱ wake, kwa maana alikuwa na wake 18 na masuria 60, naye akawazaa wana 28 na mabinti 60. **22** Kwa hiyo Rehoboamu akamweka Abiya mwana wa Maaka kuwa mkuu na kiongozi miongoni mwa ndugu zake, kwa maana alikusudia kumweka kuwa mfalme. **23** Hata hivyo, alitenda kwa

11:15 * Tnn., "mbuzi."

SURA YA 11

a 1Fa 12:31, 32

b 1Fa 13:33

c Law 17:7

d 1Fa 12:26, 28

e Kum 12:11
1Nya 22:1
2Nya 15:8, 9
2Nya 30:10, 11f 1Sa 16:6
1Sa 17:13g 2Sa 13:1
2Sa 18:33h 1Fa 15:1
2Nya 12:16
Mt 1:7

i Kum 17:17

Safu ya 2

a 2Nya 11:5, 11

SURA YA 12

b 2Nya 11:17

c Kum 32:15
2Nya 26:11, 16d 1Fa 11:40
1Fa 14:25

e Nah 3:9

f 1Fa 12:22-24

g Kum 28:15
2Nya 15:2

h 2Nya 33:10, 12

i 1Fa 21:29
2Nya 34:26, 27

busara* na kuwatuma[#] baadhi ya wanawe kwenye mae-neo yote ya Yuda na Benjamine, kwenye majiji yote yenye ngome,^a akawapa chakula kingi na kuwatafutia wake wengi.

12 Mara tu baada ya utawala wa Rehoboamu kuimarika kabisa,^b naye akawa na nguvu, aliiacha Sheria ya Yehova,^c na Waisraeli wote pia wakaiacha. **2** Katika mwaka wa tano wa utawala wa Mfalme Rehoboamu, Mfalme Shishaki^d wa Misri alishambulia Yerusalemu, kwa maana hawakuwa waaminifu kwa Yehova. **3** Alikuwa na magari 1,200 ya vita, wapanda farasi 60,000, na idadi isiyohesabika ya wanajeshi waliokuja pamoja naye kutoka Misri—Walibya, Wasukii, na Waethiopia.^e **4** Aliyateka majiji yenye ngome ya Yuda na mwishowe akafika Yerusalemu.

5 Nabii Shemaya^f akaja kwa Rehoboamu na wakuu wa Yuda waliokuwa wamekusanyika Yerusalemu kwa sababu ya Shishaki, akawaambia: "Yehova anasema hivi, 'Mmeniacha mimi, nami pia nime-waacha ninyi mikononi^g mwa Shishaki.'" **6** Ndipo wakuu wa Israeli na mfalme wakajinyenyekeza^h na kusema: "Yehova ni mwadilifu." **7** Yehova alipoona kwamba wamejinyenyekeza, neno la Yehova likamjia Shemaya likisema: "Wamejinyenyekeza. Sitawaa-ngamiza,ⁱ na baada ya muda mfupi nitawaokoa. Sitalimwagia jiji la Yerusalemu ghadhabu yangu kupitia Shishaki.

11:23 * Tnn., "uelewaji." # Au "kuwasambaza."

8 Lakini watakuwa watumishi wake, ili wajue tofauti kati ya kunitumikia mimi na kuwatumikia wafalme wa* nchi nyi-gine.”

9 Basi Mfalme Shishaki wa Misri akashambulia Yerusalemu. Akachukua hazina za nyumba ya Yehova^a na hazina za nyumba ya* mfalme. Ali-chukua kila kitu, kutia ndani ngao za dhahabu ambazo Sulemani alikuwa ametengeneza.^b 10 Basi Mfalme Rehoboamu akatengeneza ngao za shaba zichukue mahali pa ngao hizo, akaziweka chini ya ulinzi wa mkuu wa walinzi,* aliyelinda mlango wa nyumba ya mfalme. 11 Wakati wowote ambapo mfalme alikuja katika nyumba ya Yehova, walinzi waliingia ndani na kuzichukua, kisha walizirudisha katika chumba cha walinzi. 12 Kwa sababu mfalme aliji-nyenyekeza, hasira ya Yehova iliacha kuwaka dhidi yake,^c naye hakuwaangamiza kabisa.^d Isitoshe, kulikuwa na mambo fulani mema yaliyopatikana nchini Yuda.^e

13 Mfalme Rehoboamu alii-marisha mamlaka yake jijini Yerusalemu na kuendelea kutawala; Rehoboamu alikuwa na umri wa miaka 41 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 17 huko Yerusalemu, jiji ambalo Yehova alichagua miongoni mwa makabila yote ya Israeli ili kuweka jina lake humo. Mama yake alii-twa Naama, naye alikuwa Mwamoni.^f 14 Lakini alitenda maovu, kwa maana haku-

12:8 *Tnn., “kutumikia falme za.” 12:9 *Au “jumba la.” 12:10 *Tnn., “wakimbaji.”

SURA YA 12

a 1Fa 7:51

b 1Fa 10:16, 17
1Fa 14:25-28

c 2Nya 33:10, 12

d Omb 3:22

e Mwa 18:23-25
1Fa 14:1, 13
2Nya 19:2, 3f Kum 23:3
1Fa 11:1
1Fa 14:21

Safu ya 2

a 1Sa 7:3
1Fa 18:21
Mk 12:30

b 1Fa 12:22-24

c 2Nya 9:29
2Nya 13:22

d 1Fa 14:30, 31

e 2Sa 5:9

f Mt 1:7

SURA YA 13

g 1Fa 15:1, 2

h 2Nya 11:20, 21

i Yos 18:28
1Sa 10:26

j 1Fa 15:6

k 2Nya 11:1

l Mwa 49:10
2Sa 7:8
Zb 78:70, 71m 2Sa 7:12, 13
1Nya 17:11, 14
Lu 1:32

n Zb 89:28, 29

o 2Nya 10:2

p 1Fa 11:26, 27
1Fa 12:20

wa ameazimia moyoni mwake kumtafuta Yehova.^a

15 Na historia ya Rehoboamu, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, je, haijaandikwa katika maandishi ya nabii Shemaya^b na mwonaji Ido^c katika kumbukumbu za ukoo? Kulikuwa na vita daima kati ya Rehoboamu na Yeroboamu.^d 16 Kisha Rehoboamu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi;^e na Abiya^f mwanawe akawa mfalme baada yake.

13 Katika mwaka wa 18 wa utawala wa Mfalme Yeroboamu, Abiya akawa mfalme wa Yuda.^g 2 Alitawala kwa miaka mitatu huko Yerusalemu. Mama yake alii-twa Mikaya^h binti ya Urieli wa Gibea.ⁱ Na kulikuwa na vita kati ya Abiya na Yeroboamu.^j

3 Basi Abiya akaenda vitani akiwa na jeshi lenye mashujaa hodari 400,000 waliozoezwa.*^k Na Yeroboamu akajipanga kivita ili kupigana naye akiwa na wanaume 800,000, mashujaa hodari waliozoezwa.* 4 Sasa Abiya akasimama juu ya Mlima Semaraimu, katika eneo lenye milima la Efraimu, akasema: “Nisikilizeni, Ee Yeroboamu na Waisraeli wote. 5 Je, hamjui kwamba Yehova Mungu wa Israeli alimpa Daudi ufalme juu ya Israeli milele,^l yeye na wawawe,^m kupitia agano la chumvi?^{*n} 6 Lakini Yeroboamu^o mwana wa Nebati, mtumishi wa Sulemani mwana wa Daudi, akainika na kumwasi bwana wake.^p 7 Na wanau-

13:3 *Tnn., “waliochaguliwa.” 13:5 *Yaani, agano linalodumu na lisilobadilika.

me wazembe, wasiofaa kitu wakaendelea kujiunga naye. Nao walimzidi maarifa Rehoboamu mwana wa Sulemani, Rehoboamu alipokuwa kijana mchanga asiye na ujasi-ri, naye hangeweza kushindana nao.

8 “Na sasa mnafikiri kwamba mnaweza kushindana na ufalme wa Yehova ulio mikononi mwa wana wa Daudi kwa sababu ninyi ni umati mkubwa nanyi mna ndama wa dhahabu ambao Yeroboamu aliwate-ngenezea wawe miungu yenu.^a

9 Je, hamjawafukuza makuhani wa Yehova,^b wazao wa Haruni, na Walawi, na je, hamjawaweka makuhani wenu wenyewe kama yalivyofanya mataifa ya nchi nyingine?^c Yeyote aliyelea* ng’ombe dume mchanga na kondoo dume saba, angeweza kuwa kuhani wa vitu ambavyo si miungu.

10 Lakini sisi, Yehova ndiye Mungu wetu,^d nasi hatujamwacha; makuhani wetu, wazao wa Haruni, wanamhudumia Yehova, na Walawi wanawasaidia kazi. **11** Wanamfukizia Yehova moshi wa dhahabu za kuteketezwa kila asubuhi na kila jioni^e pamoja na uvumba uliotiwa manukato,^f na mikate ya tabaka*^g iko kwenye meza iliyotengenezwa kwa dhahabu safi, nao wanawasha kinara cha taa cha dhahabu^h na taa zake kila jioni,ⁱ kwa sababu tunatekeleza jukumu letu kwa Yehova Mungu wetu; lakini ninyi mmemwacha. **12** Sasa tazama! Mungu wa kweli yuko pamoja nasi, akituongoza, na makuhani

13:9 *Tnn., “aliyeujaza mkono wake na.”
13:11 *Yaani, mikate ya wonyesho.

SURA YA 13

a 1Fa 12:26, 28
2Nya 11:15

b 2Nya 11:14

c 1Fa 12:31, 33
1Fa 13:33

d 2Nya 11:16

e Kut 29:39

f Kut 30:1

g Kut 25:30

h Kut 25:31

i Kut 27:20

Safu ya 2

a Hes 10:9

b 2Nya 14:11
2Nya 18:31

c 2Fa 18:1, 5
1Nya 5:20
2Nya 16:8
Zb 22:5
Zb 37:5
Nah 1:7

d 1Fa 12:28, 29

e Yoh 11:54

f 1Sa 25:38
1Fa 14:20
Mdo 12:21-23

wake wakiwa na tarumbeta za kutoa ishara ya vita dhidi yenu. Enyi wanaume wa Israeli, msipigane na Yehova Mungu wa mababu zenu, kwa maana hamtafanikiwa.”^a

13 Lakini Yeroboamu alituma wanajeshi wawavizie kutoa nyuma, hivi kwamba jeshi lake lilikabili Yuda upande wa mbele na wanajeshi waliovizia walikuwa nyuma yao. **14** Wanaume wa Yuda walipogeeuka, waligundua kwamba wanashambuliwa kutoka mbele na nyuma. Kwa hiyo wakaanza kumlilia Yehova,^b huku makuhani wakipiga tarumbeta kwa sauti kubwa. **15** Wanaume wa Yuda wakaanza kupiga kelele za vita, na wanaume hao wa Yuda walipopiga kelele za vita, Mungu wa kweli akamshinda Yeroboamu na Waisraeli wote mbele ya Abiya na Yuda. **16** Waisraeli wakawakimbia wanaume wa Yuda, na Mungu akawatia mikononi mwao. **17** Abiya na watu wake waka wachinja wanajeshi wengi, wakaendelea kuwaua wanajeshi wa Israeli, waliwaua wanaume 500,000 waliozoezwa.* **18** Basi wanaume wa Israeli wakanyenyekezwa wakati huo, lakini wanaume wa Yuda waliwashinda kwa sababu walimtegemea* Yehova Mungu wa mababu zao.^c **19** Abiya akandelea kumfuatia Yeroboamu, akateka majiji yake, Betheli^d na miji yake, Yeshana na miji yake, na Efraini^e na miji yake. **20** Na Yeroboamu hakupata tena mamlaka* katika siku za Abiya; kisha Yehova akampiga, naye akafa.^f

13:17 *Tnn., “waliochaguliwa.” **13:18** *Tnn., “walimwegemea.” **13:20** *Tnn., “nguvu.”

21 Lakini Abiya akaendelea kupata nguvu. Baada ya muda akaoa wake 14,^a akazaa wana 22 na mabinti 16. 22 Na mambo mengine katika historia ya Abiya, mambo aliyotenda na kusema, yameandikwa katika maandishi ya* nabii Ido.^b

14 Kisha Abiya akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi;^c na Asa mwanawe akawa mfalme baada yake. Katika siku zake nchi ilikuwa na amani* kwa miaka kumi.

2 Asa alitenda yaliyokuwa mema na sawa machoni pa Yehova Mungu wake. 3 Aliondoa madhabahu za kigeni^d na mahali pa juu, akazivunjavunja nguzo takatifu,^e na kukata miti mitakatifu.*^f 4 Zaidi ya hayo, aliwaambia watu wa Yuda wamtafute Yehova Mungu wa mababu zao na kushika Sheria na amri. 5 Kwa hiyo aliondoa mahali pa juu na vinara vya uvumba^g katika majiji yote ya Yuda, na chini ya utawala wake ufalme uliendelea kuwa bila usumbufu. 6 Alijenga majiji yenye ngome huko Yuda,^h kwa kuwa nchi haikuwa na usumbufu na hakuna yeyote aliyepigana vita naye katika miaka hiyo, kwa maana Yehova alimpumzisha.ⁱ 7 Aliwaambia hivi watu wa Yuda: “Na tujenge majiji haya na kuyazingira kwa kuta na minara,^j malango* na makomeo. Kwa maana nchi bado imo mikononi mwetu kwa sababu tumemtafuta Yehova

13:22 *Au “ufafanuzi wa; maelezo ya.” 14:1 *Tnn., “ilipumzika.” 14:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 14:7 *Tnn., “mila-ngo miwili-miwili.”

SURA YA 13

a Kum 17:17

b 2Nya 9:29
2Nya 12:15

SURA YA 14

c 2Sa 5:9

d Kum 7:5

e Kut 23:24

f 1Fa 14:22, 23
2Fa 18:1, 4

g 2Nya 34:1, 4

h 2Nya 11:5

i 2Nya 15:15
Met 16:7

j 2Nya 32:2, 5

Safu ya 2

a Zb 127:1

b 2Nya 11:1, 12
2Nya 13:3

c 2Nya 16:8

d Yos 15:20, 44
2Nya 11:5, 8e Kut 14:10
1Nya 5:20
2Nya 32:20f Amu 7:7
1Sa 14:6g 2Nya 13:12
2Nya 32:7, 8h 1Sa 17:45
Zb 20:5
Met 18:10i Yos 7:9
Zb 9:19

j Kum 28:7

k Mwa 20:1

Mungu wetu. Tumemtafuta, naye ametupumzisha pande zote.” Kwa hiyo kazi yao ya ujenzi ilifanikiwa.^a

8 Asa alikuwa na jeshi la wanaume 300,000 waliokuwa na ngao kubwa na mikuki. Na kutoka Benjamini kulikuwa na mashujaa hodari 280,000 waliobeba ngao ndogo* na kujihami kwa pinde.^{#b}

9 Baadaye Zera Mwethiopia akaja kupigana nao akiwa na jeshi la wanaume 1,000,000 na magari 300 ya vita.^c Alipofika Maresha,^d 10 Asa akaenda kupigana naye, na Asa na jeshi lake wakajipanga kivita katika Bonde la Sefatha huko Maresha. 11 Kisha Asa akamlilia Yehova Mungu wake^e akisema: “Ee Yehova, haijalishi kwako ikiwa wale unao-wasaidia ni wengi au hawana nguvu.^f Tusaidie, Ee Yehova Mungu wetu, kwa maana tunakutegemea* wewe,^g na katika jina lako tumekuja kupigana na umati huu.^h Ee Yehova, wewe ni Mungu wetu. Usiache mwanadamu anayeweza kufa akushinde.”ⁱ

12 Kwa hiyo Yehova akawashinda Waethiopia mbele ya Asa na mbele ya watu wa Yuda, na Waethiopia wakakimbia.^j 13 Asa na watu waliokuwa pamoja naye wakawafuatia mpaka Gerari,^k nao wakaendelea kuwaua Waethiopia hivi kwamba hakuna hata mmoja wao aliyebaki hai, kwa maana walipondwaponywa na Yehova na jeshi lake. Kisha wakachukua nyara nyingi sana. 14 Zaidi ya hayo, wa-

14:8 *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale. #Tnn., “kukanyaga upinde.” 14:11 *Tnn., “tunakutegemea.”

liyashambulia majiji yote yaliyozunguka Gerari, kwa maana hofu ya Yehova ilikuwa imewashika wakaaji wa majiji hayo; nao wakapora majiji yote, kwa kuwa kulikuwa na vitu vingi vya kuporwa katika majiji hayo. **15** Walishambulia pia mahema ya wale waliokuwa na mifugo, wakateka idadi kubwa ya kondoo na ngamia, kisha wakarudi Yerusalemu.

15 Sasa roho ya Mungu ilimjia Azaria mwana wa Odedi. **2** Kwa hiyo akatoka kwenda kukutana na Asa, akamwambia: “Nisikilizeni, Asa na watu wote wa Yuda na Benjamini! Yehova yuko pamoja nanyi maadamu mnaendelea kuwa pamoja naye;^a nanyi mkimtafuta, atawaruhusu mumpate,^b lakini mki mwacha yeye atawaacha ninyi.^c **3** Kwa muda mrefu* Waisraeli hawakuwa na Mungu wa kweli, hawakuwa na kuhani wa kuwafundisha, na hawakuwa na sheria.^d **4** Lakini walipokuwa wakiteseka, walimrudia Yehova Mungu wa Israeli na kumtafuta, naye akawaruhusu wampate.^e **5** Siku hizo hakuna yeyote aliyeweza kusafiri akiwa salama,* kwa sababu kulikuwa na misukosuko mingi miongoni mwa wakaaji wote wa nchi mbalimbali. **6** Taifa lilikuwa likipondwa na taifa lingine na jiji likipondwa na jiji lingine, kwa sababu Mungu aliwawuruga kwa kila aina ya mateso.^f **7** Lakini ninyi, iweni imara na msivunjike moyo,^g kwa maa-

15:3 *Tnn., “siku nyingi.” 15:5 *Tnn., “hakukuwa na amani kwa yule aliyetoka nje au kuingia ndani.” 15:7 *Tnn., “msigeze mikono.”

SURA YA 15

a Yak 4:8

b Isa 55:6

c 1Nya 28:9
Ebr 10:38

d Kum 33:8, 10
2Nya 17:8, 9
Mal 2:7

e Zb 106:43, 44
Isa 55:7

f Kum 28:15, 48

g Yos 1:9
1Nya 28:20

Safu ya 2

a 2Fa 23:24

b 2Nya 8:12

c 2Nya 11:16
2Nya 30:25

d Kum 4:29
2Fa 23:3
Ne 10:28, 29

e Kut 22:20

f 2Nya 15:2

na mtapata thawabu kwa ajili ya kazi yenu.”

8 Mara tu Asa aliposikia maneno hayo na unabii wa nabii Odedi, akajipa ujasiri, akaondoa sanamu zenye kuchukiza katika nchi yote ya Yuda^a na Benjamini na katika majiji aliyokuwa ameteka katika eneo lenye milima la Efraimu, naye akajenga upya madhabahu ya Yehova iliyokuwa mbele ya ukumbi wa Yehova.^b **9** Akawakusanya pamoja watu wote wa Yuda na Benjamini na wakaaji wageni waliokuwa pamoja nao kutoka Efraimu na Manase na Simeoni,^c kwa maana walikuwa wamekimbia na kuja kwake kwa wingi kutoka Israeli walipoona kwamba Yehova Mungu wake alikuwa pamoja naye. **10** Basi wakakusanywa pamoja Yerusalemu katika mwezi wa tatu wa mwaka wa 15 wa utawala wa Asa. **11** Siku hiyo walimtolea Yehova dhambi kutoka katika nyara walizoleta, ng'ombe 700 na kondoo 7,000. **12** Zaidi ya hayo, walifanya agano ili kumtafuta Yehova Mungu wa mababu zao kwa moyo wao wote na kwa nafsi* yao yote.^d **13** Mtu yeyote ambaye hangemtafuta Yehova Mungu wa Israeli angeuawa, awe mdogo au mkubwa, awe mwanamume au mwanamke.^e **14** Basi wakamwambia Yehova kwa sauti kubwa, kwa kelele za shangwe, na kwa tarumbeta na pembe. **15** Na watu wote wa Yuda wakashangilia kwa sababu ya kiapo hicho, kwa maana walikuwa wameapa kwa moyo wao wote, walimtafuta kwa bidii naye akawaruhusu wampate,^f

15:12 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

na Yehova akaendelea kuwampumzisha pande zote.^a

16 Mfalme Asa alimwondoa hata Maaka^b nyanya yake kutoka katika cheo chake cha mama malkia, kwa sababu alikuwa ametengeneza sanamu chafu sana* kwa ajili ya ibada ya mti mtakatifu.^c Asa akai-katakata sanamu hiyo chafu sana, akaipondaponda na kuiteteza katika Bonde la Kidroni.^d **17** Lakini mahali pa juu hapakuondolewa^e Israeli.^f Hata hivyo, moyo wa Asa ulikuwa kamili* maisha yake yote.^g **18** Naye alileta kati-ka nyumba ya Mungu wa kweli vitu ambavyo yeye na baba yake walikuwa wamevifanya kuwa vitakatifu—fedha, dhahabu, na vyombo mbalimbali.^h **19** Hakukuwa na vita mpa-ka mwaka wa 35 wa utawala wa Asa.ⁱ

16 Katika mwaka wa 36 wa utawala wa Asa, Mfalme Baasha^j wa Israeli alikuja kushambulia Yuda, akaanza kujenga* Rama^k ili kumzuia mtu yeyote asitoke wala kuingia kwa* Mfalme Asa wa Yuda.^l **2** Ndipo Asa akatoa fedha na dhahabu kutoka katika hazina za nyumba ya Yehova^m na nyumba ya* mfalme na kumpelekea Mfalme Ben-hadadi wa Siria,ⁿ aliyekuwa akiishi Damasko, akamwambia: **3** “Kuna mkataba* kati yangu na wewe na kati ya baba yangu na baba yako. Ninakutumia fedha na dhahabu. Njoo,

15:16 *Yaani, kingono. ^aAngalia Kamusi, uku. 2012. 15:17 *Au “ulikuwa na ujitoaji kamili.” ^bTnn., “siku zake zote.” 16:1, 5, 6 *Au “kuimarisha; kuje-nga upya.” 16:1 *Au “asiandoke wala kuingia katika eneo la.” 16:2 *Au “ju-мба la.” 16:3 *Au “agano.”

SURA YA 15

a Met 16:7

b 1Fa 15:9,10

c Kum 13:6-9

d 1Fa 15:13,14

e 1Fa 22:43

f 1Fa 14:22,23
2Fa 14:3,4
2Fa 23:19,20

g 1Fa 8:61

h 1Fa 7:51
1Fa 15:15
1Nya 26:26

i 2Nya 14:1

SURA YA 16

j 1Fa 15:25,27

k Yos 18:21,25

l 1Fa 15:17-19

m 1Fa 7:51

n 1Fa 20:1
2Fa 12:18
2Fa 16:8

Safu ya 2

a 2Fa 15:29

b Amu 18:29

c 1Fa 15:20-22

d Yos 18:21,25
1Fa 15:17e Yos 18:21,24
1Nya 6:60,64f Yos 18:21,26
Amu 20:1g 1Fa 16:1
2Nya 19:2
2Nya 20:34

h Yer 17:5

i 2Nya 14:9,11
Zb 37:39,40

j Zek 4:10

k 1Pe 3:12

l 1Fa 15:32

vuja mkataba wako* na Mfalme Baasha wa Israeli, ili aondo-ke kwangu.”

4 Ben-hadadi akamsikiliza Mfalme Asa, akawatuma wakuu wa majeshi yake kushambulia majiji ya Israeli, wakashinda Iyoni,^a Dani,^b Abel-maimu, na maghala yote ya majiji ya Naftali.^c **5** Baasha aliposikia habari hizo, mara moja akaacha kujenga* Rama, akasimamisha kazi hiyo. **6** Kisha Mfalme Asa akawachukua watu wote wa Yuda, nao wakabeba mawe na mbao zilizokuwa zikitumiwa na Baasha kujenga Rama,^d akazitumia kujenga* Geba^e na Mispá.^f

7 Wakati huo mwonaji Hanani^g akaja kwa Mfalme Asa wa Yuda na kumwambia: “Kwa sababu ulimtegemea* mfalme wa Siria nawe hukumtegemea* Yehova Mungu wako, jeshi la mfalme wa Siria limeponyoka kutoka mikononi mwako.^h **8** Je, Waethiopia na Walibya hawakuwa jeshi kubwa sana lenye magari mengi ya vita na wapanda farasi? Lakini kwa sababu ulimtegemea Yehova, aliwatia mikononi mwako.ⁱ **9** Kwa maana macho ya Yehova yanaenda huku na huku duniani kote^j ili adhirishe nguvu zake* kwa nia-ba ya wale ambao moyo wao ni kamili* kumweleka yeye.^k Umetenda kwa upumbavu katika jambo hili; kuanzia sasa na kuendelea kutakuwa na vita dhidi yako.”^l

10 Hata hivyo, Asa akamkasirikia mwonaji huyo na ku-

16:3 *Au “agano lako.” 16:7 *Tnn., “ulimwegemea.” ^aTnn., “hukumwegemea.” 16:9 *Au “utegemezo wake.” ^bAu “una ujitoaji kamili.”

mtia gerezani,* alikasirishwa sana naye kwa sababu ya jambo hilo. Wakati huohuo, Asa akaanza kuwatesa watu wengine. **11** Sasa historia ya Asa, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, imeandikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Yuda na wa Israeli.^a

12 Katika mwaka wa 39 wa utawala wake, Asa alishikwa na ugonjwa miguuni, akawa mgonjwa sana; na hata alipokuwa mgonjwa, hakumwomba Yehova msaada, bali waponyaji. **13** Kisha Asa akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake;^b alikufa katika mwaka wa 41 wa utawala wake. **14** Kwa hiyo walimzika katika kaburi lake la kifahari alilokuwa amejichimbia katika Jiji la Daudi;^c walimlaza kwenye machela ya kubebea maiti iliyojazwa mafuta ya zeri na mafuta* yaliyotengenezwa kwa njia ya pekee kwa mchanganyiko wa vikolezo mbalimbali.^d Isitoshе, waliwasha moto mkubwa isivyo kawaida kwa ajili yake.^e

17 Na Yehoshafati^e mwana- we akawa mfalme baada yake, akaimarisha mamla- ka yake juu ya Israeli. **2** Aliweka majeshi katika majiji yote ya Yuda yenye ngome na kuweka kambi za kijeshi katika nchi ya Yuda na katika majiji ya Efraimu ambayo Asa baba yake alikuwa ameyateka.^f **3** Yehova aliendelea kuwa pamoja na Yehoshafati kwa sababu alitembea katika njia za awali za Daudi babu yake^g naye hakutafuta Maba-

16:10 *Tnn., "katika nyumba ya mikatale." **16:14** *Au "marhamu." [#]Inaonekana kwamba hawakuichoma maiti ya Asa, bali walichoma vikolezo vyenye manukato.

SURA YA 16

a 1Fa 15:23

b 1Fa 15:24

c 2Sa 5:7

d Mk 16:1
Lu 23:55, 56
Yoh 19:40

SURA YA 17

e 1Fa 15:24
1Fa 22:41

f 2Nya 15:8

g 2Sa 8:15

Safu ya 2

a Kum 4:29
2Nya 26:1, 5b 1Fa 12:28-30
1Fa 13:33c 1Fa 9:4, 5
Zb 132:12

d 2Nya 18:1

e 1Fa 22:42, 43

f Kum 7:5

g Kum 33:8, 10
Mal 2:7h Kum 31:11
Yos 1:7, 8
Ne 8:7

i 2Nya 18:1

j 2Nya 14:2, 6

k 1Fa 9:19
2Nya 8:3, 4

li. **4** Kwa maana alimtafuta Mungu wa baba yake^a na kufuata* amri yake wala si mazoea ya Waisraeli.^b **5** Yehova aliendelea kuuimarisha kabisa ufalme mikononi mwake;^c na watu wote wa Yuda wakaeendelea kumpa Yehoshafati zawadi, akawa na utajiri na utukufu mwingi.^d **6** Moyo wake ukawa jasiri katika njia za Yehova, na hata aliondoa mahali pa juu^e na miti mitakatifu*^f huko Yuda.

7 Katika mwaka wa tatu wa utawala wake aliwaita wakuu wake, yaani, Ben-haili, Obadia, Zekaria, Nethaneli, na Mikaya, ili wafundishe katika majiji ya Yuda. **8** Walikuwa pamoja na Walawi wafuatao: Shemaya, Nethania, Zebadia, Asaheli, Shemiramothi, Yehonathani, Adoniya, Tobaya, na Tobadoniya, pamoja na kuhani Elishama na kuhani Yehoram.^g **9** Walianza kufundisha nchini Yuda, wakiwa na kitabu cha Sheria ya Yehova,^h nao walizunguka katika majiji yote ya Yuda wakiwafundisha watu.

10 Na falme zote katika nchi zilizozunguka Yuda zikashikwa na hofu ya Yehova, nazo hazikumshambulia Yehoshafati. **11** Wafilisti wakamletea Yehoshafati zawadi na pesa kama ushuru. Waarabu wakamletea kondoo dume 7,700 na mbuzi dume 7,700 kutoka katika makundi yao.

12 Yehoshafati akaendelea kuwa mkuu zaidi na zaidi,ⁱ akaendelea kujenga ngome^j na majiji yenye maghala^k huko Yuda. **13** Alitekeleza miradi mikubwa katika

17:4 *Tnn., "kutembea katika." **17:6** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

majiji ya Yuda, naye alikuwa na wanajeshi, mashujaa hodari, Yerusalemu. **14** Wali-pangwa kulingana na koo zao:* mkuu wa maelfu katika ukoo wa Yuda alikuwa mkuu Adna, naye alikuwa na mashujaa hodari 300,000.^a **15** Na mkuu Yehohanani alikuwa chini ya amri yake, naye alikuwa na mashujaa hodari 280,000. **16** Na pia Amasia mwana wa Zikri aliyejitolea kwa ajili ya utumishi wa Yehova alikuwa chini ya amri yake, naye alikuwa na mashujaa hodari 200,000. **17** Na kutoka katika ukoo wa Benjamini,^b kulikuwa na Eliada, shujaa hodari, naye alikuwa na wanau-me 200,000 waliokuwa na pinde na ngao.^c **18** Na Yehozabadi alikuwa chini ya amri yake, naye alikuwa na wanau-me 180,000 waliokuwa tayari kwa ajili ya vita. **19** Wanau-me hao walikuwa wakimhudumia mfalme pamoja na wale ambao mfalme aliwaweka katika majiji yenye ngome kote-kote nchini Yuda.^d

18 Yehoshafati alikuwa na utajiri na utukufu mwingi,^e lakini alifanya mapatano ya ndoa pamoja na Ahabu.^f **2** Basi miaka kadhaa baadaye alishuka kwenda kwa Ahabu kule Samaria,^g na Ahabu akamtotea yeye na watu waliokuwa pamoja naye dhahabu ya kondoo na ng'ombe wengi. Naye akamhimiza* apande kwenda kushambulia Ramothi-gileadi.^h **3** Kisha Mfalme Ahabu wa Israeli akamuuliza Mfalme Yehoshafati wa Yuda: “Je, utaenda pamoja

17:14 * Yaani, ukoo wa upande wa baba.
18:2 * Au “akamshawishi.”

SURA YA 17

a 2Nya 13:3
2Nya 26:11-13

b Mwa 49:27

c 2Nya 14:8

d 2Nya 11:5, 23

SURA YA 18

e 2Nya 17:5

f 1Fa 16:28, 33
1Fa 21:25

g 1Fa 22:2-4
2Nya 19:2

h Kum 4:41-43
1Nya 6:77, 80

Safu ya 2

a 2Sa 2:1
1Fa 22:5, 6

b 2Fa 3:11

c 1Fa 22:7, 8

d 1Fa 18:4
1Fa 19:9, 10

e Yer 38:4

f 1Fa 22:9-12

nami Ramothi-gileadi?” Akamjibu: “Mimi ni kama wewe, na watu wangu ni kama watu wako, nao watakuunga mkono vitani.”

4 Lakini Yehoshafati akamwambia mfalme wa Israeli: “Tafadhali, kwanza tafuta neno la Yehova.”^a **5** Kwa hiyo mfalme wa Israeli akawakusanya pamoja manabii, wanau-me 400, akawauliza: “Je, twende kupigana vita dhidi ya Ramothi-gileadi, au nisiende?” Wakasema: “Panda uende, na Mungu wa kweli atalitia jiji hilo mikononi mwako mfalme.”

6 Kisha Yehoshafati akasema: “Je, hakuna nabii wa Yehova mahali hapa?”^b Acheni tumuulize yeye pia.”^c **7** Ndi-po mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: “Bado kuna mtu mmoja^d ambaye tunaweza kumwomba ushauri kutoka kwa Yehova; lakini ninamchukia, kwa maana hatabiri kamwe mambo mema kunihusu, anatabiri mabaya sikuzote.^e Anaitwa Mikaya mwana wa Imla.” Hata hivyo, Yehoshafati akasema: “Mfalme, usiseme jambo kama hilo.”

8 Basi mfalme wa Israeli akamwita ofisa fulani wa makao ya mfalme na kumwambia: “Mete haraka Mikaya mwana wa Imla.”^f **9** Sasa mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda walikuwa wameketi kila mmoja wao kwenye kiti chake cha ufalme, akiwa amevaa mavazi ya kifalme, katika uwanja wa kupuria nafaka kwenye lango la kuingia Samaria, na manabii wote walikuwa wakitabiri mbele yao. **10** Kisha Sedekia mwana wa Kenaana akajitengenezea pembe za chuma

na kusema: “Yehova anasema hivi: ‘Kwa pembe hizi utawapiga* Wasiria mpaka utakapowaangamiza.’” **11** Wale manabii wengine wote walikuwa wakitabiri vivyo hivyo, wakisema: “Panda mpaka Ramothigileadi, nawe utafanikiwa;^a Yehova atalitia jiji hilo mikononi mwako mfalme.”

12 Basi mjumbe aliyeenda kumwita Mikaya akamwambia: “Tazama! Manabii wote kwa pamoja wanasema mema kumhusu mfalme. Tafadhali, acha neno lako liwe kama maneno yao,^b useme mema.”^c

13 Lakini Mikaya akasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, jambo lolote ambalo Mungu wangu atasema ndilo nitakalosema.”^d

14 Kisha akaingia kwa mfalme, naye mfalme akamuuliza: “Mikaya, je, twende kupigana vita dhidi ya Ramothigileadi, au nisiende?” Mara moja akajibu: “Panda uende nawe utafanikiwa; watatiwa mikononi mwako.” **15** Ndipo mfalme akamuuliza: “Nitakupaisha mara ngapi kwamba hupaswi kuniambia jambo lingine lolote isipokuwa ukweli katika jina la Yehova?” **16** Basi Mikaya akasema: “Ninawaona Waisraeli wote wakiwa wame-tawanyika milimani, kama kondoo wasio na mchungaji.^e Yehova akasema: ‘Hawa hawana bwana. Acha kila mmoja wao arudi kwa amani nyumbani kwake.’”

17 Kisha mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: “Je, sikukwambia, ‘Hatatabiri mambo mema kunihusu, ila mabaya?’^f

SURA YA 18

a Mik 3:5

b Isa 30:9,10

c 1Fa 22:13-17

d Yer 23:28
Mdo 20:27e Law 26:14, 17
Hes 27:16, 17

f 1Fa 22:18

Safu ya 2

a Isa 6:1
Eze 1:26
Ufu 20:11b Ayu 1:6
Da 7:9, 10

c 1Fa 22:19-23

d Zb 104:4

e Isa 19:14
Eze 14:9

f 2Nya 18:10

g 2Nya 18:7

h Yer 20:2
Mk 14:65

i 1Fa 22:24-28

18 Ndipo Mikaya akasema: “Basi, sikia neno la Yehova: Nilimwona Yehova akiwa ameketi kwenye kiti chake cha ufalme^a na jeshi lote la mbinguni^b likiwa lime-simama upande wake wa kulia na upande wake wa kushoto.^c **19** Halafu Yehova akauliza, ‘Ni nani atakayemdanganya Mfalme Ahabu wa Israeli, ili apande kwenda na kufia huko Ramothigileadi?’ Na malaika mmoja akasema jambo moja na mwingine akasema jambo lingine. **20** Kisha roho*^d fulani akaja na kusimama mbele za Yehova na kusema, ‘Mimi nitamdanganya.’ Yehova akamuuliza, ‘Utatumia njia gani?’ **21** Akajibu, ‘Nitaenda na kuwa roho ya udanganyifu katika vinywa vya manabii wake wote.’ Kwa hiyo akasema, ‘Utamdanganya, na zaidi ya hilo, utafanikiwa. Nenda ukafanye hivyo.’ **22** Na sasa Yehova ametia roho ya udanganyifu katika vinywa vya hawa manabii wako,^e lakini Yehova ametangaza kwamba utapata msiba.”

23 Sasa Sedekia^f mwana wa Kenaana akamkaribia Mikaya^g na kumpiga kwenye shavu^h na kumuuliza: “Roho ya Yehova iliniacha jinsi gani na kuja kuzungumza nawe?”ⁱ **24** Mikaya akamjibu: “Tazama! Utajua ni jinsi gani utakapoingia katika chumba cha ndani zaidi kujificha.” **25** Ndipo mfalme wa Israeli akasema: “Mchukue Mikaya umpeleke kwa Amoni mkuu wa jiji na kwa Yoashi mwana wa mfalme. **26** Waambie, ‘Mfalme anasema hivi:

18:10 *Au “utawasukuma.”

18:20 *Au “malaika.”

“Mfungeni mtu huyu gerezani^a na kumlisha kiasi kidogo cha mkate na maji mpaka nitakaporudi kwa amani.””²⁷ Lakini Mikaya akasema: “Ukirusudi kwa amani, basi Yehova hajazunguma nami.”^b Kisha akasema: “Zingatieni maneno yangu, enyi watu wote.”

28 Basi mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda wakapanda kwenda Ramothi-gileadi.^c **29** Ndipo mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: “Nitabadili sura yangu na kuingia vitani, lakini wewe vaa mavazi yako ya kifalme.” Kwa hiyo mfalme wa Israeli akabadili sura yake, nao wakalingia vitani. **30** Sasa mfalme wa Siria alikuwa amewaagiza hivi makamanda wake wa magari ya vita: “Msipigane na yeyote, mdogo au mkubwa, isipokuwa mfalme wa Israeli.” **31** Na mara tu makamanda hao wa magari ya vita walipomwona Yehoshafati, wakambiana: “Ni mfalme wa Israeli.” Basi wakamgeukia ili kupigana naye; na Yehoshafati akaanza kulilia msaada,^d na Yehova akamsaidia, na mara moja Mungu akawaelekeza upande mwingine ili wamwache. **32** Makamanda hao wa magari ya vita walipoona kwamba hakuwa mfalme wa Israeli, mara moja wakaacha kumfuatia.

33 Lakini mtu fulani alivuta upinde wake bila kukusudia* na kumpiga mfalme wa Israeli katikati ya sehemu ambazo koti lake la vita linaungana. Basi mfalme akamwambia mtu aliyeesha gari lake: “Geu-

18:33 *Au “bila nia mbaya.”

SURA YA 18

a 2Nya 16:10
Mdo 5:18

b Hes 16:29

c Yos 20:8
1Fa 22:29-33
2Nya 18:2

d Kut 14:10
2Nya 13:14

Safu ya 2

a 1Fa 22:34, 35

b 2Nya 18:22

SURA YA 19

c 2Nya 18:31, 32

d 1Fa 16:1

e 2Nya 16:7

f 1Fa 21:25

g Zb 139:21

h 1Fa 14:1, 13

i 2Nya 17:3-6

j Yos 17:14, 15

k 2Nya 15:8

l Kum 16:18

m Kum 1:16, 17
Zb 82:1

ka uniondoe vitani,* kwa sababu nimejeruhiwa vibaya.”^a **34** Vita vikapamba moto siku hiyo yote, nao wakalazimika kumsimamisha mfalme ndani ya gari, akiwaelekea Wasiria mpaka jioni; akafa jua lilipokuwa likitua.^b

19 Kisha Mfalme Yehoshafati wa Yuda akarudi salama salimini^c katika nyumba yake* huko Yerusalemu. **2** Yehu^d mwana wa mwonaji Hanani^e alienda kukutana na Mfalme Yehoshafati na kumuuliza: “Je, unapaswa kuwasaidia waovu,^f na je, unapaswa kuwapenda wale wanaomchukia Yehova?^g Kwa sababu hiyo ghadhabu ya Yehova iko dhidi yako. **3** Hata hivyo, kuna mambo mema ambayo yamepatikana ndani yako,^h kwa sababu uliiondoa kabisa miti mitakatifu* nchini, nawe umeutayarisha moyo wakoⁱ kumtufuta Mungu wa kweli.”ⁱ

4 Yehoshafati akaendelea kuishi Yerusalemu, naye akatoka tena na kwenda kukutana na watu kuanzia Beersheba mpaka kwenye eneo lenye milima la Efraimu,^j ili awarudishe kwa Yehova Mungu wa mababu zao.^k **5** Pia, aliwaweka waamuzi katika nchi yote, katika majiji yote ya Yuda yenye ngome, jiji baada ya jiji.^l **6** Akawaambia hivi waamuzi: “Iweni waangalifu kuhusu mambo mnyayotenda, kwa maana hamhukumu kwa ajili ya mwanadamu bali kwa ajili ya Yehova, naye yupo pamoja nanyi mnapotoa hukumu.^m **7** Basi hofu ya Ye-

18:33 *Tnn., “kambini.” 19:1 *Au “jumba lake la kifalme.” 19:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au “na moyo wako umeazimia.”

hova na iwe juu yenu.^a Iweni waangalifu kuhusu mambo mnyotenda, kwa maana Yehova Mungu wetu hana ukosefu wa haki,^b hana ubaguzi,^c wala hapokei rushwa.”^d

8 Pia huko Yerusalemu, Yehoshafati aliwaweka baadhi ya Walawi na makuhani na baadhi ya viongozi wa koo* za Waisraeli watumikie wakiwa waamuzi kwa ajili ya Yehova na kusuluhisha kesi za wakaaji wa Yerusalemu.^e

9 Akawaamuru: “Hivi ndivyo mnavyopaswa kufanya huku mkimwogopa Yehova, kwa uaminifu na kwa moyo kamili:*

10 Kila mara ndugu zenu wanaoishi katika majiji yao wakiwaletea kesi inayohusu umwagaji wa damu^f au swali kuhusu sheria fulani, amri, masharti, au maamuzi, mnapaswa kuwaonya ili wasiwe na hatia mbele za Yehova; msipofanya hivyo ghadhabu yake itakuja dhidi yenu na dhidi ya ndugu zenu. Hivyo ndivyo mnavyopaswa kufanya ili msiwe na hatia. **11** Ndiye huyu Amaria mkuu wa makuhani anayewasimamia katika kila jambo linalomhusu Yehova.^g Zebadia mwana wa Ishmaeli ndiye kiongozi wa ukoo wa Yuda katika kila jambo linalomhusu mfalme. Na Walawi watatumikia wakiwa maofisa wenu. Iweni imara, na mte nde, na Yehova awe pamoja na wale wanaotenda mema.”^{*h}

20 Baadaye Wamoabuⁱ na Waamoni,^j pamoja na baadhi ya Waamonimu,* wakaja kupigana vita na Yeho-

19:8 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.
19:9 *Au “moyo wenye ujitoaji kamili.”
19:11 *Au “awe na kilicho chema.” 20:1
*Au labda, “Wameuni.”

SURA YA 19

a Kut 18:21

b Mwa 18:25
Kum 32:4c Mdo 10:34
Ro 2:11
1Pe 1:17d Kum 10:17
Kum 16:19e Kum 17:9
Kum 21:5
Kum 25:1

f Kum 17:8

g Mal 2:7

h 2Nya 15:2

SURA YA 20

i Amu 3:14
2Sa 8:2
Zb 83:2, 6

j Mwa 19:36-38

Safu ya 2

a Yos 15:1

b Yos 15:20, 62

c 2Nya 19:1, 3

d Kum 4:29-31

e 1Fa 8:23
Mt 6:9f 1Nya 29:11
Da 4:17g 1Nya 29:12
Isa 40:15, 17
Da 4:35h Mwa 12:7
Ne 9:7, 8
Isa 41:8
Yak 2:23

i 2Nya 2:4

j 2Nya 6:20

shafati. **2** Basi Yehoshafati akaambiwa hivi: “Umami mku-bwa umekuja kukushambulia kutoka katika eneo la bahari,* kutoka Edomu,^a wamefika Hasason-tamari, yaani, Engedi.”^b **3** Ndipo Yehoshafati akaogopa, akaazimia* kumtafuta Yehova.^c Basi akatanga za watu wote wa Yuda wafunge. **4** Kisha watu wa Yuda wakakusanyika pamoja kuta-futa ushauri wa Yehova;^d walikuja kutoka katika majiji yote ya Yuda ili kutafuta ushauri wa Yehova.

5 Ndipo Yehoshafati akasi-mama katika kutaniko la Yuda na Yerusalemu ndani ya nyumba ya Yehova mbele ya ule ua mpya, **6** akasema:

“Ee Yehova Mungu wa mababu zetu, je, wewe si Mungu mbinguni;^e je, huna mamlaka juu ya falme zote za mataifa?^f Mkononi mwako mna nguvu na uwezo, na hakuna anayeweza kushindana nawe.^g **7** Ee Mungu wetu, je, hukuwafukuza wakaaji wa nchi hii kuto-ka mbele ya watu wako Waisraeli na kisha kuupa uzao wa* rafiki yako Abrahamu nchi hii iwe miliki yao ya kudumu?^h

8 Nao wakaishi katika nchi hiyo na kukujengea humo mahali patakatifu kwa ajili ya jina lako,ⁱ wakisema, **9** “Tukipatwa na msiba, upanga, hukumu kali, au ugonjwa hata-ri, au njaa, na tusimame mbele ya nyumba hii na mbele zako (kwa maana jina lako limo katika nyumba hii)/ na kukulilia utusaidie katika taabu yetu, nawe usikie na

20:2 *Inaonekana ni Bahari ya Chumvi.
20:3 *Tnn., “akauuelekeza uso wake.”
20:7 *Tnn., “mbegu ya.”

kutuokoa.^a **10** Sasa tazama, ndio hawa wanaume wa Amoni, Moabu, na eneo lenye milima la Seiri,^b ambao hu-kuwaruhusu Waisraeli wawavamie walipotoka nchini Misiri. Waligeuka na kwenda mbali nao na hawakuwaangamiza.^c **11** Sasa wanatulipa kwa kuja kutufukuza kutoka katika miliki yako uliyotupatia iwe urithi wetu.^d **12** Ee Mungu wetu, je, hutatekeza hukumu dhidi yao?^e Kwa maana hatuna nguvu mbele ya umati huu mkubwa unaokuja kutushambulia; nasi hatujui tunalopaswa kufanya,^f lakini macho yetu yanakutazama wewe.^g

13 Wakati huo, watu wote wa Yuda walikuwa wamesimama mbele za Yehova, pamoja na watoto wao wadogo, wake zao, na wana wao.

14 Ndipo katikati ya kutaniko, roho ya Yehova ikamjia Yahazieli mwana wa Zekaria mwana wa Benaya mwana wa Yeieli mwana wa Matania, Mlawi wa wana wa Asafu. **15** Akasema: "Sikilizeni kwa makini, enyi watu wote wa Yuda nanyi wakaaji wa Yerusalemu na Mfalme Yehoshafati! Yehova anawaambia hivi: 'Msiogope wala msihofu kwa sababu ya umati huu mkubwa, kwa maana vita si vyenu bali ni vya Mungu.^h **16** Kesho shukeni kukabiliana nao. Watakuwa wakipanda kupitania ya Sisi, nanyi mtawakuta mwishoni mwa bonde* kabla ya nyika ya Yerueli. **17** Hamtahitaji kupigana vita hivi. Simameni mahali penu, simameni tuli,ⁱ muuone wokovu wa

20:16 * Au "korongo."

SURA YA 20

a 1Fa 8:33, 34
2Nya 6:28-30

b Mwa 36:8

c Hes 20:17, 18
Kum 2:5, 9, 19

d Amu 11:23, 24
Zb 83:2, 4

e Amu 11:27, 28
Zb 7:6

f 2Fa 6:15, 16

g 2Nya 14:11
Zb 25:15
Zb 62:1

h Kum 1:29, 30
Yos 11:4, 6
2Nya 32:7, 8

i Isa 30:15

Safu ya 2

a Kut 14:13, 14
Kut 15:2
1Sa 2:1
1Nya 16:23
Omb 3:26

b Kum 31:8
Yos 10:25

c Hes 14:9
2Nya 15:2

d 1Nya 23:12

e 1Nya 15:16

f 2Nya 11:5, 6

g Kut 14:31
Kut 19:9

h 1Nya 15:16

i Kut 34:6

j Amu 7:22
1Sa 14:20

Yehova kwa ajili yenu.^{*a} Enyi watu wa Yuda na Yerusalemu, msioogope wala msihofu.^b Kesho nendeni mkakabili nani, na Yehova atakuwa pamoja nanyi.^{”c}

18 Mara moja Yehoshafati akainama chini kifudifudi, na watu wote wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu wakaanguka chini mbele za Yehova ili kumwabudu Yehova. **19** Kisha Walawi waliokuwa wazao wa Wakohathi^d na wazao wa Wakora wakasimama ili kumsifu Yehova Mungu wa Israeli kwa sauti kubwa sana.^e

20 Kesho yake, wakaamka asubuhi na mapema na kwenda katika nyika ya Tekoa.^f Walipokuwa wakienda, Yehoshafati akasimama na kusema: "Nisikilizeni, enyi watu wa Yuda nanyi wakaaji wa Yerusalemu! Iweni na imani katika Yehova Mungu wenu ili mweze kusimama imara.* Iweni na imani katika manabii wake,^g nanyi mtafanikiwa.[”]

21 Baada ya kushauriana na watu, aliwaweka wanaume ili wamwimbie^h Yehova na kumsifu wakiwa wamevaa mavazi matakatifu huku wakiwatangulia wanaume wenye silaha, wakisema: "Mshukuruni Yehova, kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.^{”i}

22 Walipoanza kuimba kwa shangwe nyimbo za sifa, Yehova akawaweka watu wawavizie wanaume wa Amoni, Moabu, na eneo lenye milima la Seiri waliokuwa wakiwamia Yuda, nao wakaangamizana wenyewe kwa wenyewe.^j

20:17 * Au "muone jinsi Yehova atakavyowaokoa." 20:20 * Au "kuvumilia."

23 Na Waamoni na Wamoabu wakageuka na kuwashambulia wakaaji wa eneo lenye milima la Seiri^a ili wawaue na kuwaangamiza kabisa; na baada ya kuwamaliza wakaaji wa Seiri, wakasaidiana kuangamizana wao kwa wao.^b

24 Lakini watu wa Yuda walipofika kwenye mnara wa mlinzi wa nyikani^c na kutazama umati huo, waliona maiti zao zikiwa zimetapakaa ardhi; ^d hakuna yeyote aliyeponyoka. **25** Basi Yehoshafati na watu wake wakaja kuchukua nyara kutoka kwao, wakapata vitu vingi sana, mavazi, na vitu vyenye kutamanika, ambavyo waliwavua mpaka waliposhindwa kubeba zaidi.^e Walichukua nyara hizo kwa siku tatu, kwa maana zilikuwa nyingi sana. **26** Siku ya nne walikusanyika pamoja katika Bonde la* Beraka, kwa maana walimsifu^f Yehova huko. Ndiyo sababu tangu siku hiyo walipaita mahali hapo Bonde la Beraka.^{Δf}

27 Kisha watu wote wa Yuda na Yerusalemu, wakiongozwa na Yehoshafati, wakarudi Yerusalemu wakishangilia, kwa maana Yehova alikuwa amefanya washangilie dhidi ya maadui wao.^g **28** Basi wakaingia Yerusalemu wakiwa na vinanda, vinubi,^h na tarumbetaⁱ na kwenda katika nyumba ya Yehova.^j **29** Na falme zote za nchi mbalimbali ziliposikia kwamba Yehova alikuwa amepigana na maadui wa Israeli zilishikwa na hofu ya Mungu.^k **30** Kwa hiyo ufalme wa Yehoshafati haukuwa na usumbufu

SURA YA 20

a Kum 2:5

b Kut 14:25
Eze 38:21

c 2Nya 20:16

d Kut 14:30
Zb 110:5, 6
Isa 37:36

e Kut 12:35
2Fa 7:15, 16

f Kut 17:14, 15
1Sa 7:12

g 1Sa 2:1
Zb 20:5
Zb 30:1

h 2Sa 6:5
1Nya 16:5

i Hes 10:8
1Nya 13:8
2Nya 29:26

j Zb 116:19

k Kut 15:13, 14
Yos 9:3, 9
2Nya 17:10

Safu ya 2

a Yos 23:1
2Sa 7:1
2Nya 15:15

b 1Fa 22:41, 42

c 1Fa 15:11

d 2Nya 17:3, 4
2Nya 19:2, 3

e 1Fa 15:14
1Fa 22:43
2Nya 17:1, 6

f 1Fa 18:21

g 1Fa 16:1
2Nya 19:2

h 2Nya 16:7

i 2Fa 1:2, 16

j 1Fa 10:22, 23

k Hes 33:1, 35
Kum 2:8
1Fa 9:26

l 2Nya 19:2
Zb 127:1

m 1Fa 22:48

SURA YA 21

n 1Fa 22:50

wowote, na Mungu wake akaendelea kumpumzisha pande zote.^a

31 Na Yehoshafati akaendelea kutawala Yuda. Alikuwa na umri wa miaka 35 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 25 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Azuba binti ya Shilhi.^b **32** Aliendelea kutembea katika njia ya Asa baba yake.^c Hakugeuka kutoka katika njia hiyo, naye alitenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova.^d **33** Hata hivyo, mahali pa juu hapakuondolewa,^e na bado watu hawakuwa wameutayarisha moyo wao kwa ajili ya Mungu wa mababu zao.^f

34 Na mambo mengine katika historia ya Yehoshafati, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, yameandikwa katika maandishi ya Yehu^g mwana wa Hanani,^h yaliyotiwa katika Kitabu cha Wafalme wa Israeli. **35** Baada ya hayo Mfalme Yehoshafati wa Yuda akaungana na Mfalme Ahazia wa Israeli, aliyetenda uovu.ⁱ **36** Kwa hiyo akashirikiana naye katika kutengeneza meli za kwenda Tarshishi,^j walizitengezeza kule Esion-geberi.^k **37** Hata hivyo, Eliezeri mwana wa Dodavahu wa Maresha alitoa unabii dhidi ya Yehoshafati, akisema: “Kwa sababu umeungana na Ahazia, Yehova ataharibu kazi zako.”^l Basi meli hizo zikavunjika,^m kwa hiyo hazikuweza kwenda Tarshishi.

21 Kisha Yehoshafati akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi; na Yehoram mwana-
we akawa mfalme baada yake.ⁿ

20:26 *Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.” #Tnn., “walimbariki.” ΔMaana yake “Baraka.”

2 Ndugu zake, yaani, wana wa Yehoshafati, walikuwa Azaria, Yehieli, Zekaria, Azaria, Mikaeli, na Shefatia; hao wote walikuwa wana wa Mfalme Yehoshafati wa Israeli. 3 Na baba yao alikuwa amewapa zawadi nyingi za fedha na dhahabu, na vitu vyenye thamani, pamoja na majiji yenye ngome kule Yuda;^a lakini alimpa Yehoram ufalme,^b kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mzaliwa wa kwanza.

4 Yehoram alipochukua mamlaka ya ufalme wa baba yake, aliimarisha mamlaka yake kwa kuwaua ndugu zake wote^c kwa upanga, na pia baadhi ya wakuu wa Israeli. 5 Yehoram alikuwa na umri wa miaka 32 alipoanza kutawala, naye alitawala huko Yerusalemu kwa miaka minane.^d 6 Alitembea katika njia ya wafalme wa Israeli,^e kama walivyofanya watu wa nyumba ya Ahabu, kwa maana alikuwa amemwoa binti ya Ahabu;^f na Yehoram akaendelea kutenda maovu machoni pa Yehova. 7 Lakini Yehova hakutaka kuiangamiza nyumba ya Daudi kwa sababu ya agano alilokuwa amefanya pamoja na Daudi,^g kwa maana alikuwa ameahidi kumpa taa, yeye na wanawe, sikuzote.^h

8 Katika siku zake, Waedomu waliasi nchi ya Yudaⁱ na kujichagulia mfalme wao wenyewe.^j 9 Basi Yehoram na makamanda wake wakavuka na magari yake yote ya vita, naye akaondoka usiku na kuwashinda Waedomu waliokuwa wamemzingira yeye na makamanda wake wa magari ya vita. 10 Lakini tangu siku hiyo Waedomu wameendelea

SURA YA 21

a 2Nya 11:5, 23

b 2Fa 8:16

c Amu 9:5, 6

d 2Fa 8:17-19

e 1Fa 14:7,9
Ho 4:1f 2Nya 22:2
Ne 13:26g 2Sa 23:5
Zb 89:20, 28
Yer 33:20, 21h 2Sa 7:12, 16
1Fa 11:36
Zb 132:11

i Mwa 27:40

j 1Fa 22:47
2Fa 8:20-22

Safu ya 2

a Yos 21:13
2Fa 19:8b 2Nya 15:2
Yer 2:13

c Kum 12:2

d 2Fa 2:1, 11

e 2Nya 17:3

f 1Fa 15:11
2Nya 14:2, 5

g 1Fa 16:25, 33

h Kut 34:15
Yer 3:8

i 2Fa 9:22

j 2Nya 21:4

k 1Fa 11:14
2Nya 33:11
Isa 10:5l Yos 13:1, 2
2Sa 8:1

m 2Nya 17:11

n 1Fa 14:25, 26

kuiasi nchi ya Yuda. Watu wa Libna^a pia walimwasi Yehoram wakati huo, kwa sababu alikuwa amemwacha Yehova Mungu wa mababu zake.^b 11 Alikuwa amejenga pia mahali pa juu^c kwenye milima ya Yuda, akasababisha wakaaji wa Yerusalemu wafanye ukahaba wa kiroho, naye akawapotosha watu wa Yuda.

12 Baadaye alipokea barua kutoka kwa nabii Eliya^d iliyo-sema: "Yehova Mungu wa Daudi babu yako anasema, 'Hujafuata* njia za Yehoshafati baba yako^e wala njia za Mfalme Asa^f wa Yuda. 13 Lakini unafuata njia ya wafalme wa Israeli^g na kusababisha watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu wafanye ukahaba wa kiroho^h kama ukahaba uliofan-nywa na nyumba ya Ahabu,ⁱ na hata uliwaua ndugu zako mwenyewe,^j watu wa nyumba ya baba yako, waliokuwa bora kuliko wewe. 14 Kwa hiyo, Yehova anawaletea pigo kubwa watu wako, wana wako, wake zako, na mali zako zote. 15 Nawe utashikwa na magonjwa mengi, kutia ndani ugonjwa wa matumbo, mpaka ugonjwa huo utakaposababisha matumbo yako yatoke nje, siku baada ya siku.'"

16 Kisha Yehova akawachoea^{*k} Wafilistiⁱ na Waarabu^m walioishi karibu na Wae-thiopia ili wamshambulie Yehoram. 17 Basi wakai-vamia Yuda, wakaingia humo kwa nguvu na kuchukua mali zote zilizokuwa katika nyumba ya* mfalme,ⁿ na pia wa-

21:12 *Tnn., "Hujatembea katika."

21:16 *Tnn., "akaichochea roho ya."

21:17 *Au "jumba la."

nawe na wake zake; Yehohazi,*^a mwanawe wa mwisho, ndiye mwana pekee aliyebaki pamoja naye. **18** Na baada ya mambo hayo yote, Yehova akampiga kwa ugonjwa wa matumbo usioweza kupona.^b **19** Wakati fulani baadaye, baada ya miaka miwili kamili kupita, matumbo yake yalitoka nje kwa sababu ya ugonjwa huo, naye akafa alipokuwa akiteseka sana kwa sababu ya ugonjwa huo; na watu wake hawakuwasha moto kwa ajili yake kama ule uliowashwa kwa ajili ya mababu zake.^c **20** Alikuwa na umri wa miaka 32 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 8 huko Yerusalemu. Hakuna mtu yote aliyesikitishwa na kifo chake. Basi wakamzika katika Jiji la Daudi,^d lakini si katika makaburi ya wafalme.^e

22 Kisha wakaaji wa Yerusalemu wakamweka Ahazia mwanawe wa mwisho kuwa mfalme baada yake, kwa maana kundi la wavamizi lililokuja kambini pamoja na Waarabu lilikuwa limewaua wana wote wakubwa wa Yehoram.^f Kwa hiyo Ahazia mwana wa Yehoram akaanza kutawala akiwa mfalme wa Yuda.^g **2** Ahazia alikuwa na umri wa miaka 22 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa mwaka mmoja huko Yerusalemu. Mama yake alitwa Athalia^h mjukuu wa* Omri.ⁱ

3 Yeye pia alitembea katika njia za nyumba ya Ahabu,^j kwa maana mama yake alikuwa mshauri wake katika kutenda maovu. **4** Naye

21:17 * Anaitwa pia Ahazia. 22:2 * Tnn., "binti ya."

SURA YA 21

a 2Nya 22:1

b Mdo 12:21-23

c 2Nya 16:13, 14
Yer 34:4, 5

d 1Fa 2:10

e 2Nya 24:24, 25
2Nya 28:27

SURA YA 22

f 2Nya 21:16, 17

g 2Fa 8:24-26

h 2Fa 11:1
2Fa 11:13, 16
2Nya 24:7

i 1Fa 16:28

j 1Fa 16:33
2Fa 8:27, 28
Mik 6:16

Safu ya 2

a 2Fa 8:15
2Fa 10:32b 1Fa 22:3
2Nya 18:14

c Yos 19:18, 23

d 2Fa 9:15

e 2Fa 8:16

f 2Fa 3:1

g 2Fa 9:16

h 1Fa 19:16
2Fa 9:20, 21

i 2Fa 9:6, 7

j 2Fa 10:10-14

k 2Fa 9:27, 28

aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, kama watu wa nyumba ya Ahabu, kwa maana walikuwa washauri wake baada ya kifo cha baba yake, jambo lililofanya aangamie. **5** Alifuata ushauri wao, akaenda pamoja na Yehoram mwana wa Mfalme Ahabu wa Israeli kupigana vita na Mfalme Hazaeli^a wa Siria kule Ramothi-gileadi,^b ambako wapiga-mishale wali-mjeruhi Yehoram. **6** Akarudi Yezreeli^c ili apone majeraha aliyopata kule Rama alipopigana na Mfalme Hazaeli wa Siria.^d

Ahazia* mwana wa Yehoram^e mfalme wa Yuda alishuka kwenda Yezreeli kumwona Yehoram^f mwana wa Ahabu, kwa sababu alikuwa amejeruhiwa.^g **7** Lakini Mungu alisababisha Ahazia aangamie alipokuja kwa Yehoram; na alipokuja, alienda pamoja na Yehoram kukutana na Yehu^h mjukuu* wa Nimshi, ambaye Yehova alikuwa amemia mafuta ili awaangamize kabisa watu wa nyumba ya Ahabu.ⁱ **8** Yehu alipoanza kutekeleza hukumu dhidi ya watu wa nyumba ya Ahabu, aliwapata wakuu wa Yuda na pia wana wa ndugu za Ahazia, wahu-dumu wa Ahazia, akawau.^j **9** Kisha akamtafuta Ahazia; wakamkamata mahali alipokuwa akijificha kule Samaria na kumleta kwa Yehu. Halafu wakamuua na kumzika,^k kwa maana walisema: "Yeye ni mjukuu wa Yehoshafati, aliyemtafuta Yehova kwa

22:6 * Anaitwa "Azaria," katika baadhi ya hati za Kiebrania. ^aAu "alikuwa mgonjwa." 22:7 * Tnn., "mwana."

moyo wake wote.”^a Hapakuwa na mtu yeyote wa nyumba ya Ahazia aliyekuwa na mamlaka ya kutawala ufalme huo.

10 Athalia,^b mama ya Ahazia, alipoona kwamba mwana-wake amekufa, alitoka na kuingamiza uzao wote wa kifalme* wa nyumba ya Yuda.^c

11 Hata hivyo, Yehoshabeathi binti ya mfalme alimchukua Yehoashi^d mwana wa Ahazia, akamwiba kutoka miongoni mwa wana wa mfalme waliopaswa kuuawa na kumweka yeye pamoja na mlezi wake katika chumba cha ndani cha kulala. Yehoshabeathi binti ya Mfalme Yehoram^e (alikuwa mke wa kuhani Yehoyada^f na dada ya Ahazia) alifanikiwa kumficha ili Athalia asimwone, kwa hiyo hakumuua.^g **12** Akakaa pamoja nao kwa miaka sita, akiwa amefichwa katika nyumba ya Mungu wa kweli Athalia alipokuwa akiitawala nchi.

23 Katika mwaka wa saba, Yehoyada alitenda kwa ujasiri na kufanya mapatano* na wakuu wa mamia,^h yaani, Azaria mwana wa Yerohamu, Ishmaeli mwana wa Yehohananani, Azaria mwana wa Obedi, Maaseya mwana wa Adaya, na Elishafati mwana wa Zikri. **2** Kisha wakazunguka katika nchi yote ya Yuda na kuwakusanya pamoja Walawiⁱ kutoka katika majiji yote ya Yuda na viongozi wa koo* za Waisraeli. Walipofika Yerusalemu, **3** kutaniko lote lilifanya agano^j pamoja na mfalme katika nyumba ya Mungu wa kweli, kisha akawaambia:

22:10 *Tnn., “mbegu yote ya ufalme.”
23:1 *Au “agano.” 23:2 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 22

a 2Nya 17:3, 4

b 2Nya 22:2

c 2Fa 11:1-3

d 2Fa 11:21

e 2Fa 8:16

f 2Nya 23:1

g 2Sa 7:12, 13
1Fa 15:4
2Nya 21:7

SURA YA 23

h 2Fa 11:4

i 2Nya 8:14

j 2Sa 5:3

Safu ya 2

a 2Sa 7:8, 12
1Fa 2:4
1Fa 9:5
Zb 89:20, 29

b 1Nya 24:3

c 2Fa 11:5-8
1Nya 9:22-25
1Nya 26:1

d 1Fa 7:1

e 1Fa 7:12

f 1Nya 23:28, 32

g 2Fa 11:9-12

h 1Nya 24:1
1Nya 26:1

i 2Fa 11:4

j 2Sa 8:7

“Tazama! Mwana wa mfalme atatawala, kama Yehova alivyoahidi kuhusu wana wa Daudi.^a **4** Hivi ndivyo mtakavyofanya: Theluthi moja ya makuhani na ya Walawi watakaoshika zamu^b siku ya Sabato watalinda malango;^c **5** na theluthi nyingine watakuwa katika nyumba ya* mfalme,^d na theluthi nyingine watakuwa katika Lango la Msingi, na watu wote watakuwa katika nyua za nyumba ya Yehova.^e **6** Msimruhusu mtu yeyote aingie katika nyumba ya Yehova isipokuwa makuhani na Walawi wanaohudumu.^f Hao wanaweza kuingia kwa sababu ni kikundi kitakatifu, na watu wote watatimiza wajibu kwa Yehova. **7** Walawi wanapaswa kumzunguka mfalme pande zote, kila mmoja akiwa na silaha zake mikononi mwake. Yeyote atakayeingia katika nyumba hiyo atauawa. Mfuateni mfalme popote aendapo.”*

8 Walawi na watu wote wa Yuda wakafanya sawasawa na alivyoamuru kuhani Yehoyada. Basi kila mmoja wao akachukua wanaume wake walio-kuwa na zamu siku ya Sabato, pamoja na wale ambao hawakuwa na zamu siku ya Sabato,^g kwa maana kuhani Yehoyada hakuwa ameviruhusu vikundi^h vilivyoshika zamu viondoke. **9** Kisha kuhani Yehoyada akawapa wakuu wa mamiaⁱ miku-ki na ngao ndogo* na ngao za mviringo zilizokuwa za Mfalme Daudi,^j ambazo zilikuwa

23:5 *Au “jumba la.” 23:7 *Tnn., “anapotoka nje na anapoingia ndani.” 23:9 *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale.

katika nyumba ya Mungu wa kweli.^a **10** Halafu akawaweka watu wote, kila mmoja akiwa na silaha yake mkononi, kuanzia upande wa kulia wa nyumba mpaka upande wa kushoto wa nyumba, kando ya madhabahu na kando ya nyumba hiyo, kumzunguka mfalme pande zote. **11** Kisha wakamtoa nje mwana wa mfalme^b na kumvika taji na Ushahidi,^{*c} wakamweka kuwa mfalme, ndipo Yehoyada na wana-we wakamtia mafuta. Halafu wakasema: “Mfalme na aishi muda mrefu!”^d

12 Athalia aliposikia sauti ya watu wakikimbia na kumsifu mfalme, mara moja akaja na kujiunga na watu katika nyumba ya Yehova.^e **13** Kisha akamwona mfalme akiwa amesimama hapo karibu na nguzo ya mfalme karibu na lango. Wakuu^f na wapiga tarumbeta walikuwa na mfalme, na watu wote nchini walikuwa wakishangilia^g na kupiga tarumbeta, na waimbaji wakiwa na ala za muziki waliongoza katika kutoa sifa. * Ndi-po Athalia akayararua mavazi yake na kupaza sauti: “Ni njama! Ni njama!” **14** Lakini kuhani Yehoyada akawatoa nje wakuu wa mamia, wale walio- wekwa kulisimamia jeshi, akawaambia: “Mwondoeni miongoni mwa vikosi, na yeyote akimfuata, muueni kwa upanga!” Kwa maana kuhani alikuwa amesema: “Msimuue ndani ya nyumba ya Yehova.” **15** Basi wakamkamata, na alipofika njia ya kuingia kati-

23:11 *Labda ni kitabu cha kukunjwa kilichokuwa na Sheria ya Mungu. 23:13 *Au “walitoa ishara ya kutoa sifa.”

SURA YA 23

a 1Nya 26:26, 27
2Nya 5:1

b 2Fa 11:2

c Kum 17:18

d 1Sa 10:1, 24

e 2Fa 11:13-16

f 2Nya 23:1

g 1Fa 1:39, 40

Safu ya 2

a 2Fa 11:17, 18
2Nya 34:1, 31

b 2Fa 10:27, 28

c Kum 12:3
2Nya 34:1, 4

d Kum 13:5
1Fa 18:40

e 1Nya 23:6
1Nya 23:30, 31

f Kut 29:38
Hes 28:2

g 1Nya 9:26
1Nya 26:1, 13

h 2Fa 11:9

i 1Fa 7:7

j 2Fa 11:19, 20

ka Lango la Farasi la nyumba ya* mfalme, mara moja wakamuua hapo.

16 Kisha Yehoyada akafanya agano kati yake na watu wote na mfalme, kwamba waenda kuwa watu wa Yehova.^a **17** Baada ya hayo, watu wote wakaenda kwenye nyumba ya Baali na kuibomoa,^{*b} wakavunja vipandevipande madhabahu zake na sanamu zake,^c nao wakamuua Matani kuhani wa Baali^d mbele ya madhabahu. **18** Kisha Yehoyada akaweka usimamizi wa nyumba ya Yehova mikononi mwa makuhani na Walawi, ambao Daudi alikuwa amewapanga katika vikundi wahudumu katika nyumba ya Yehova na kutoa dhabihu za kutekelezwa za Yehova^e kulingana na yale yaliyoandikwa katika Sheria ya Musa,^f wakishangilia na kuimba, kama alivyoagiza* Daudi. **19** Aliwaweka pia walinzi wa malango^g karibu na malango ya nyumba ya Yehova, ili mtu yeyote asiye safi kwa njia yoyote ile asiingie. **20** Kisha akawachukua wakuu wa mamia,^h watu mashuhuri, watawala wa watu, na watu wote nchini, wakamsindikiza mfalme kushuka kutoka katika nyumba ya Yehova. Halafu wakaja katika nyumba ya* mfalme kupitia lango la juu na kumweka mfalme kwenye kitiⁱ cha ufalme.^j **21** Basi watu wote nchini wakashangilia na jiji likatulia, kwa maana walikuwa wamemuua Athalia kwa upanga.

23:15, 20 *Au “jumba la.” 23:17 *Au “hekalu la Baali na kulibomoa.” 23:18 *Tnn., “kwa mikono ya.”

24 Yehoashi alikuwa na umri wa miaka saba alipoanza kutawala,^a naye alitawala kwa miaka 40 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Sibia kutoka Beer-sheba.^b **2** Yehoashi aliendelea kute nda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova sikuzote za kuhani Yehoyada.^c **3** Yehoyada alimchagulia wake wawili, naye akazaa wana na mabinti.

4 Baadaye Yehoashi alitamani moyoni mwake kuirekebisha nyumba ya Yehova.^d **5** Kwa hiyo akawakusanya makuhani na Walawi na kuwambia: "Nendeni kwenye majiji ya Yuda mkusanye kutoka kwa Waisraeli wote pesa za kurekebisha nyumba ya Mungu^e mwaka baada ya mwaka; nanyi mnapaswa kushughulikia jambo hili haraka." Lakini Walawi hawakulishughulikia jambo hilo haraka.^f **6** Kwa hiyo, mfalme akamwita mkuu Yehoyada na kumuuliza:^g "Kwa nini hukuwaamuru Walawi walete kutoka Yuda na Yerusalemu kodi takatifu iliyoagizwa na Musa^h mtumishi wa Yehova, ile kodi takatifu ya kutaniko la Israeli, kwa ajili ya hema la Ushahidi?ⁱ **7** Kwa maana wana wa Athalia,^j yule mwanamke mwovu, walikuwa wamevunja na kuingia ndani ya nyumba ya Mungu wa kweli,^k nao walikuwa wametumia vitu vyote vitakatifu vya nyumba ya Yehova kwa ajili ya Mabaali."^l **8** Kisha, kwa agizo la mfalme, sanduku^m lilitengenezwa na kuwekwa nje kwenye lango la nyumba ya Yehova.ⁿ **9** Halafu tangazo likatolewa katika nchi yote ya Yuda na Yerusalemu kwamba watu wamletee Yehova kodi takatifuⁿ

SURA YA 24

a 2Fa 11:21

b Mwa 21:14
2Sa 3:10
2Fa 12:1

c 2Fa 12:2

d 2Fa 22:3-5

e 2Fa 12:4, 5
2Nya 29:1, 3
2Nya 34:9, 10

f 2Fa 12:6

g 2Fa 12:7

h Kut 30:12-16

i Hes 1:50

j 2Nya 22:2, 3

k 2Nya 28:24

l Mk 12:41

m 2Fa 12:9

n Kut 30:12-16
Ne 10:32
Mt 17:24

Safu ya 2

a 1Nya 29:9

b 2Fa 12:10

c 2Fa 12:11, 12
2Nya 34:10, 11d Kut 37:16
Hes 7:84

ambayo Musa mtumishi wa Mungu wa kweli alikuwa ame-waagiza Waisraeli nyikani. **10** Wakuu wote na watu wote wakashangilia,^a nao wakae-ndelea kuleta michango na kuitumbukiza katika sanduku hilo mpaka lilipojaa.*

11 Kila mara Walawi wali-poleta sanduku hilo ili mfalme akabidhiwe, na maofisa wali-poona kwamba kulikuwa na pesa nyingi ndani yake, mw-ndishi wa mfalme na mwaki-lishi wa kuhani mkuu waliku-ja na kuzitoa pesa sanduku-ni,^b kisha walilirudisha mahali pake. Hivyo ndivyo walivyo-fanya siku baada ya siku, nao walikusanya pesa nyingi.

12 Kisha mfalme pamoja na Yehoyada waliwapa wale waliosimamia kazi katika utu-mishi wa nyumba ya Yehova, na wasimamizi hao waliwaja-iri watu waliokata mawe na mafundi wa kurekebisha nyumba ya Yehova,^c na pia ma-fundi wa chuma na shaba ili kuirekebisha nyumba ya Yehova. **13** Na wasimamizi hao wakaianzisha kazi, na kazi hiyo ya kurekebisha ikasonga mbele chini ya usimamizi wao, nao wakairudisha nyumba ya Mungu wa kweli katika hali yake inayofaa na kuiimarisha. **14** Na mara tu walipomaliza, walimletea mfalme na Yehoya-da pesa zilizobaki, nao waka-zitumia kutengeneza vyombo vya nyumba ya Yehova, vyombo vya huduma na vya kutolea dhabihu na vikombe na vyombo vya dhahabu na vya fedha.^d Nao walitoa kwa ukawaida dhabihu za kuteke-

24:10 * Au labda, "wote walipokuwa wa-metoa."

tezwa^a katika nyumba ya Yehova sikuzote za Yehoyada.

15 Yehoyada alizeeka na kufa baada ya kuishi maisha marefu na yenye kuridhisha; alikuwa na umri wa miaka 130 alipokufa. **16** Basi wakamzika katika Jiji la Daudi pamoja na wafalme,^b kwa sababu alikuwa ametenda mema katika Israeli^c kwa ajili ya Mungu wa kweli na nyumba Yake.

17 Baada ya kifo cha Yehoyada, wakuu wa Yuda walikuja na kumwinamia mfalme, na mfalme akawasikiliza. **18** Waliacha nyumba ya Yehova Mungu wa mababu zao na kuanza kuabudu miti mitakatifu* na sanamu, hivi kwamba hasira ya Mungu ikaja[#] dhidi ya Yuda na Yerusalemu kwa sababu ya hatia yao. **19** Aliendelea kuwatuma manabii miongoni mwao ili wawarudishe kwa Yehova, nao waliendelea kuwaonya* lakini walikataa kusikiliza.^d

20 Roho ya Mungu ikamjia* Zekaria mwana wa kuhani Yehoyada,^e naye akasimama mahali palipo juu mbele ya watu na kuwaambia: "Mungu wa kweli anasema hivi: 'Kwa nini mnazivunja amri za Yehova? Hamtafanikiwa! Kwa sababu mmemwacha Yehova, yeye naye, atawaacha ninyi.'"^f **21** Lakini walipanga njama dhidi yake,^g wakampiga mawe katika ua wa nyumba ya Yehova, kwa agizo la mfalme.^h **22** Kwa hiyo Mfalme Yehoashi hakukumbuka upendo mshikamanifu ambao Yehoya-

24:18 *Angalia Kamusi, uku. 2012. [#]Tnn., "kulikuwa na hasira." **24:19** *Au "kutoa ushahidi dhidi yao." **24:20** *Au "ikamfunika."

SURA YA 24

a Hes 28:3

b 1Fa 2:10

c 2Nya 23:1

d 2Fa 17:13, 14
2Nya 36:15, 16
Yer 7:25, 26

e 2Nya 23:11

f Kum 29:24, 25
1Nya 28:9
2Nya 15:2

g Yer 11:19

h Mt 23:35
Lu 11:51

Safu ya 2

a Mwa 9:5
Zb 94:1
Yer 11:20
Ebr 10:30

b 2Fa 12:17

c 2Nya 24:17, 18

d Law 26:17, 37
Kum 32:30

e 2Nya 24:20, 21

f 2Fa 12:20

g 2Sa 5:9
1Fa 2:10h 2Nya 21:16, 20
2Nya 28:27

i 2Fa 12:21

j 2Nya 24:20

da baba yake* alimtendea, alimua mwanawe, ambaye alisema hivi alipokuwa akifa: "Yehova na ashughulikie jambo hili na kukulipiza kisasi."^a

23 Mwanzoni mwa mwaka, jeshi la Siria lilikuja kumshambulia Yehoashi, likavamia Yuda na Yerusalemu.^b Kisha likawaua wakuu wote^c wa watu na kupeleka nyara zao zote kwa mfalme wa Damasko.

24 Kwa maana ingawa jeshi la Wasiria lililovamia lilikuwa na wanaume wachache, Yehova alitia mikononi mwao jeshi kubwa sana la watu wa Yuda na Yerusalemu^d kwa sababu walikuwa wamemwacha Yehova Mungu wa mababu zao; kwa hiyo wakatekeleza* hukumu dhidi ya Yehoashi. **25** Na walipoondoka katika nchi yake (kwa maana walimwacha akiwa amejeruhiwa vibaya*), watumishi wake mwenyewe walipanga njama dhidi yake kwa sababu alikuwa amemwaga damu ya wana[#] wa kuhani Yehoyada.^e Walimua katika kitanda chake mwenyewe.^f Basi akafa na kuzikwa katika Jiji la Daudi,^g lakini hawakumzika katika makaburi ya wafalme.^h

26 Hawa ndio waliopanga njamaⁱ dhidi yake: Zabadi mwana wa Shimeathi mwana-mke Mwamoni na Yehozabadi mwana wa Shimrithi mwana-mke Mmoabu. **27** Na kuhusu wanawe na mambo mengi yaliyotangazwa dhidi yake/ na pia kazi ya kurekebisha* nyumba ya Mungu wa

24:22 *Yaani, baba ya Zekaria. **24:24** *Yaani, Wasiria. **24:25** *Au "akiwa na magonjwa mengi." [#]Au "mwana." Hue nda wingi unaonyesha utukufu. **24:27** *Tnn., "kuweka msingi wa."

kweli,^a mambo hayo yote ya-meandikwa katika maandishi ya* Kitabu cha Wafalme. Na Amazia mwanawe akawa mfalme baada yake.

25 Amazia alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 29 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Yehoadani wa Yerusalemu.^b **2** Aliendelea kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova, lakini si kwa moyo kamili. **3** Mara tu ufalme ulipoimarika kabisa mikononi mwake, aliwaua watumishi wake waliomuua mfalme, baba yake.^c **4** Lakini hakuwaua wana wao, kwa maana alitenda kulingana na mambo yaliyoandikwa katika Sheria, katika kitabu cha Musa, ambamo Yehova aliamuru hivi: "Akina baba hawapaswi kuuawa kwa sababu ya wana wao, na wana hawapaswi kuuawa kwa sababu ya baba zao; lakini kila mtu anapaswa kuuawa kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe."^d

5 Na Amazia akawakusanya pamoja watu wa Yuda na kuwaagiza wasimame kulingana na koo zao,* chini ya wakuu wa maelfu na chini ya wakuu wa mamia kwa ajili ya watu wote wa Yuda na Benjamini.^e Akawaandikisha waliokuwa na umri wa miaka 20 na zaidi,^f akapata kwamba walikuwa mashujaa 300,000 waliozozwa^g kwa ajili ya utumishi wa kijeshi, walioweza kutumia mkuki na ngao kubwa. **6** Isitoshe, alikodi mashujaa hodari 100,000 kuto-

24:27 *Au "ufafanuzi wa; maelezo ya."
25:5 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.
"Tnn.," waliochaguliwa."

SURA YA 24

a 2Nya 24:13

SURA YA 25

b 2Fa 14:1-6

c 2Nya 24:26

d Kum 24:16

e 1Sa 8:11,12

f Hes 1:2, 3

Safu ya 2

a 2Nya 19:2

b 2Nya 14:11
2Nya 20:6

c 1Sa 2:7
Met 10:22
Hag 2:8

d 2Sa 8:13
Zb 60:Uta

e 2Fa 14:7
2Nya 20:10,11

f 2Nya 25:9

ka Israeli kwa talanta 100 za fedha.* **7** Lakini mtu fulani wa Mungu wa kweli akamjia na kumwambia: "Ee mfalme, usiruhusu jeshi la Israeli liende pamoja nawe, kwa maana Yehova hayuko pamoja na Waisraeli,^a hayuko pamoja na Mwefraimu yeyote. **8** Lakini nenda peke yako, utende, na uwe jasiri vitani. Usipofanya hivyo, Mungu wa kweli anaweza kukufanya ujikwae mbele ya adui, kwa maana Mungu ana nguvu za kusaidia^b na za kusababisha mtu ajikwae." **9** Ndipo Amazia akamuuliza hivi mtu wa Mungu wa kweli: "Lakini vipi kuhusu zile talanta 100 ambazo nimewapa wanajeshi wa Israeli?" Mtu wa Mungu wa kweli akamjibu: "Yehova anaweza kukuipa nyingi zaidi kuliko hizo."^c **10** Basi Amazia akawaagiza wanajeshi waliokuwa wamekuja kwake kutoka Efraimu waende zao, warudi kwao. Hata hivyo, waliwakasirikia sana watu wa Yuda, basi wakarudi kwao wakiwa wamekasirikia sana.

11 Kisha Amazia akajipa ujasiri na kuwaongoza wanajeshi wake mwenyewe kwenye Bonde la Chumvi,^d akawaua wanaume 10,000 wa Seiri.^e **12** Na wanaume wa Yuda wakawateka watu 10,000 wakiwa hai. Wakawapandisha juu ya mwamba na kuwatupa chini kutoka kwenye mwamba huo, na wote wakavunjika vipandevipande. **13** Lakini wanajeshi ambao Amazia aliwaambia warudi, wasiende pamoja naye vitani,^f walikuwa wakivamia

25:6 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

majiji ya Yuda, kuanzia Samaria^a mpaka Beth-horoni;^b waliwaua watu 3,000 katika majiji hayo na kuchukua nyara nyingi sana.

14 Lakini Amazia aliporudi baada ya kuwaua Waedomu, alileta miungu ya watu wa Seiri na kuisimamisha ili iwe miungu yake mwenyewe,^c naye akaanza kuinama mbele ya miungu hiyo na kuifukizia moshi wa dhabihu.

15 Kwa hiyo Yehova akamkasirikia sana Amazia, akamtuma nabii ambaye alimwambia: "Kwa nini unaifuata miungu ya mataifa ambayo haikuwao-koa watu wake kutoka mikononi mwako?"^d **16** Nabii huyo alipokuwa akizungumza naye, mfalme akamwambia: "Je, tulikuweka uwe mshauri wa mfalme?"^e Nyamaza!^f Kwa nini unataka kuuawa?" Ndio nabii huyo akanyamaza, lakini akasema: "Najua kwamba Mungu ameamua kukuangamiza, kwa sababu umetenda hivyo na hujasikiliza ushauri wangu."^g

17 Baada ya kushauriana na washauri wake, Mfalme Amazia wa Yuda alituma ujumbe kwa Yehoashi mwana wa Yehoahazi mwana wa Yehu mfalme wa Israeli akisema: "Njoo, tupambane vitani."^h

18 Mfalme Yehoashi wa Israeli akatuma ujumbe huu kwa Mfalme Amazia wa Yuda: "Gugu lenye miiba kule Lebanoni lilituma ujumbe huu kwa mwerezi huko Lebanoni, 'Mpe mwanangu binti yako awe mke wake.' Hata hivyo, mnyama wa mwituni wa Lebanoni akapita karibu na kulikanyagakanyaga gugu hilo lenye miiba.

25:17 *Au "tukutane uso kwa uso."

SURA YA 25

a 1Fa 16:29

b 2Nya 8:3, 5

c Kut 20:3, 5
Kum 7:25
2Nya 28:22, 23d 2Nya 24:20
Zb 115:8
Yer 2:5
Yer 10:5e 2Nya 16:10
2Nya 18:25, 26

f Isa 30:10

g 1Sa 2:25
Met 29:1

h 2Fa 14:8-10

Safu ya 2

a 2Nya 25:11

b 2Fa 14:11-14

c 2Nya 22:7

d 2Nya 25:14

e Yos 21:8, 16
1Sa 6:19f Ne 8:16
Ne 12:38, 39g 2Nya 26:9
Yer 31:38
Zek 14:10h 1Fa 7:51
1Fa 15:18
2Fa 24:12, 13
2Fa 25:13-15
2Nya 12:9

i 2Fa 14:1

19 Umeseema, "Tazama! Nime-waangamiza Waedomu."^a Kwa hiyo moyo wako umekuwa na kiburi, unataka utukuzwe. Lakini sasa kaa katika nyumba yako mwenyewe.* Kwa nini utafute msiba kisha uanguke, na kuwaangusha pia watu wa Yuda?"

20 Lakini Amazia hakisikiliza,^b kwa sababu Mungu wa kweli alikusudia kuwata mikononi mwa adui,^c kwa sababu walikuwa wameifuata miungu ya Edomu.^d **21** Basi Mfalme Yehoashi wa Israeli akapanda kwenenda huko, naye akapambana vitani na Mfalme Amazia wa Yuda huko Beth-shemeshi,^e jiji la Yuda. **22** Watu wa Yuda wakashindwa na Waisraeli, kwa hiyo kila mmoja akakimbilia nyumbani kwake.* **23** Mfalme Yehoashi wa Israeli akamkamata Mfalme Amazia wa Yuda, mwana wa Yehoashi mwana wa Yehoahazi,* huko Beth-shemeshi. Kisha akamleta Yerusalemu, naye akabomoa ukuta wa Yerusalemu kuanzia Lango la Efraimu^f mpaka Lango la Pembeni,^g urefu wa mikono 400.^h **24** Akachukua dhahabu yote na fedha na vitu vyote vilivyokuwa katika nyumba ya Mungu wa kweli chini ya Obed-edomu na katika hazina za nyumba ya* mfalme,^h na pia akachukua mateka. Kisha akarudi Samaria.

25 Amaziaⁱ mwana wa Yehoashi mfalme wa Yuda aliendelea kuishi kwa miaka 15

25:19 *Au "jumba lako mwenyewe la kifalme." 25:22 *Tnn., "katika hema lake." 25:23 *Anaitwa pia Ahazia. #Karibu mita 178 (futi 584). Angalia Nyongeza B14. 25:24 *Au "jumba la."

baada ya kifo cha Yehoashi^a mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli.^b **26** Na mambo mengine katika historia ya Amazia, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, je, hayajaa-ndikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Yuda na wa Israeli? **27** Kuanzia wakati ambapo Amazia aligeuka na kuacha kumfuata Yehova, walipanga njama^c dhidi yake huko Yerusalemu, akakimbilia Lakishi, lakini wakawatuma watu wamfuatie huko Lakishi, nao wakamua huko. **28** Kwa hiyo wakambeba juu ya farasi na kumrudisha, wakamzika pamoja na mababu zake katika jiji la Yuda.

26 Kisha watu wote wa Yuda wakamchukua Uzia,^d aliyekuwa na umri wa miaka 16, wakamweka kuwa mfalme baada ya Amazia baba yake.^e **2** Alijenga upya jiji la Elothi^f na kulirudisha kwa Yuda baada ya mfalme* kuzikwa pamoja na mababu zake.^g **3** Uzia^h alikuwa na umri wa miaka 16 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 52 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Yekolia wa Yerusalemu.ⁱ **4** Aliendelea kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova, kama Amazia baba yake alivyotenda.^j **5** Naye aliendelea kumtafuta Mungu katika siku za Zekaria, aliyemfundisha kumwogopa Mungu wa kweli. Wakati alipokuwa aki-mtafuta Yehova, Mungu wa kweli alimfanikisha.^k

6 Alienda kupigana na Wafilisti^l na kuupenya ukuta wa Gathi,^m ukuta wa Yabne,ⁿ na ukuta wa Ashdodi.^o Kisha

26:2 *Yaani, Amazia baba yake.

SURA YA 25

a 2Fa 13:10

b 2Fa 14:17-20

c 2Fa 12:20
2Fa 15:8,10
2Fa 21:23

SURA YA 26

d Mt 1:8

e 2Fa 14:21

f 1Fa 9:26
2Fa 16:6

g 2Fa 14:22

h Isa 1:1
Isa 6:1

i 2Fa 15:2

j 2Fa 14:1, 3

k 2Nya 14:7
Zb 1:2, 3l 2Sa 8:1
2Nya 21:16
Isa 14:29

m 1Nya 18:1

n Yos 15:11, 12

o Yos 15:20, 46
1Sa 5:1

Safu ya 2

a 2Nya 17:11

b Mwa 19:36, 38
Amu 11:15

c 2Nya 14:2, 7

d 2Fa 14:13
Yer 31:38
Zek 14:10

e Ne 3:13

f 2Fa 9:17

g Hes 1:2, 3
2Sa 24:9

h 2Nya 24:11

i 2Nya 11:1
2Nya 13:3
2Nya 14:8
2Nya 17:14
2Nya 25:5

akajenga majiji katika eneo la Ashdodi na miongoni mwa Wafilisti. **7** Mungu wa kweli aliendelea kumsaidia kuwashinda Wafilisti, Waarabu^a waliokuwa wakiishi Gurbaali, na Wameunimu. **8** Waamoni^b wakaanza kumpa Uzia ushuru. Hatimaye umaarufu wake ukaenea mpaka Misri, kwa maana alipata nguvu nyingi sana. **9** Isitoshe, Uzia alijenga minara^c Yerusalemu karibu na Lango la Pembeni,^d Lango la Bondeni,^e na Nguzo ya Kutegemeza Ukuta, naye akaiimarisha. **10** Pia, alijenga minara^f nyikani na kuchimba* matangi mengi ya maji (kwa maana alikuwa na mifugo mingi sana); alifanya hivyo pia katika Shefela na katika nchi tambarare ya juu. Alikuwa na wakulima na watunzaji wa mizabibu milimani na kule Karmeli, kwa maana alipenda kilimo.

11 Zaidi ya hayo, Uzia akawa na jeshi lililolijhami kwa ajili ya vita. Wanajeshi hao walienda vitani, wakiwa wamepangwa katika vikundi. Walihesabiwa na kuandikishwa^g na mwandishi Yeieli^h na ofisa aliyetitwa Maaseya, chini ya amri ya Hanania, mmoja wa wakuu wa mfalme. **12** Idadi kamili ya viongozi wa koo* walio-waongoza mashujaa hao hodari ilikuwa 2,600. **13** Wanajeshi waliokuwa chini ya amri yao walikuwa 307,500, wanau-me waliokuwa tayari kwa ajili ya vita, jeshi lenye nguvu la kumsaidia mfalme kupigana na maadui.ⁱ **14** Uzia alili-

26:10 *Inaelekea alichimba kwenye miamba. 26:12 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

hami jeshi lote kwa ngao, mikuki,^a kofia, makoti ya vita,^b pinde, na mawe ya kombeo.^c **15** Pia, alitengeneza mitambo ya vita huko Yerusalemu iliyo-buniwa na wahandisi; iliwekwa kwenye minara^d na kwenye pembe za kuta, nayo ilikuwa na uwezo wa kurusha mishale na mawe makubwa. Basi umaarufu wake ukaenea kwa mapana na marefu, kwa maana alisaidiwa sana akawa na nguvu.

16 Hata hivyo, mara tu alipokuwa na nguvu, moyo wake ukawa na kiburi ambacho kilisababisha aangamie, naye alikosa kutenda kwa uaminifu kumwelekea Yehova Mungu wake kwa kuwa aliingia katika hekalu la Yehova ili kufukiza uvumba kwenye madhabahu ya uvumba.^e **17** Mara moja kuhani Azaria na makuhani wengine 80 wa Yehova wenye ujasiri wakamfuata humo. **18** Wakamkabili Mfalme Uzia na kumwambia: "Si vyema kwako, Uzia, kumfukiza Yehova uvumba!^f Ni makuhani tu wanaopaswa kufukiza uvumba, kwa maana wao ni wazao wa Haruni,^g waliotakaswa. Toka mahali patakati-fu, kwa maana hujatenda kwa uaminifu, na kwa sababu hiyo hutapokea utukufu wowote kutoka kwa Yehova Mungu."

19 Lakini Uzia, aliyekuwa ameshika chetezo mkononi, akawaka hasira;^h na hasira yake ilipokuwa imewaka dhidi ya makuhani, ukomaⁱ ukatokea kwenye paji lake la uso mbele ya makuhani katika nyumba ya Yehova karibu na madhabahu ya uvumba. **20** Azaria mkuu wa makuhani na makuhani wote walipogeuka na kumtazama, walio-

SURA YA 26

a 2Nya 11:5, 12

b 1Sa 17:4, 5

c Amu 20:16
1Sa 17:49
1Nya 12:1, 2

d 2Nya 14:2, 7

e Hes 1:51

f Hes 16:39, 40
Hes 18:7g Kut 30:7
1Nya 23:13h 2Nya 16:10
2Nya 25:15, 16i Hes 12:10
2Fa 5:27

Safu ya 2

a Law 13:45, 46
Hes 5:2
Hes 12:14, 15

b 2Fa 15:5-7

c Isa 1:1
Isa 6:1

d 2Fa 15:32

SURA YA 27

e Isa 1:1
Ho 1:1
Mik 1:1
Mt 1:9

f 2Fa 15:33

g 2Fa 15:34, 35
2Nya 26:3, 4

h 2Nya 26:16-18

i Yer 26:10

j 2Nya 33:1, 14
Ne 3:26k 2Nya 11:5
2Nya 14:2, 7

na kwamba alikuwa amepigwa na ukoma kwenye paji la uso! Kwa hiyo wakamtoa humo haraka, naye mwenyewe akatoka nje haraka, kwa sababu Yehova alikuwa amemletea pigo.

21 Mfalme Uzia aliendelea kuwa na ukoma mpaka siku aliyokufa, naye aliendelea kukaa katika nyumba iliyotengwa akiwa mtu mwenye ukoma,^a kwa sababu alizuiwa kuingia katika nyumba ya Yehova. Yothamu mwanawe ndiye aliyesimamia nyumba ya* mfalme, akiwahukumu watu nchini.^b

22 Na mambo mengine katika historia ya Uzia, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, yaliandikwa na nabii Isaya^c mwana wa Amози. **23** Kisha Uzia akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake, lakini alizikwa katika kiwanja cha kuzikia kilichokuwa mali ya wafalme, kwa maana walisema: "Ni mtu mwenye ukoma." Na Yothamu mwanawe^d akawa mfalme baada yake.

27 Yothamu^e alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 16 huko Yerusalemu. Mama yake alii-twa Yerusha binti ya Sadoki.^f **2** Aliendelea kutenda yali-yokuwa sawa machoni pa Yehova, kama alivyotenda Uzia baba yake,^g ila tu hakingia kwa nguvu katika hekalu la Yehova.^h Lakini bado watu walikuwa wakitenda maovu. **3** Alijenga lango la juu la nyumba ya Yehova,ⁱ naye alifanya kazi kubwa ya ujenzi kwenye ukuta wa Ofeli.^j **4** Alijenga pia majiji^k katika eneo

26:21 *Au "jumba la."

lenye milima la Yuda,^a akajenga ngome^b na minara^c misituni. **5** Alipigana vita na mfalme wa Waamoni^d na hatimaye akawashinda, hivi kwamba mwaka huo Waamoni wakampa talanta 100 za fedha,* kori 10,000 za ngano,[#] na 10,000 za shayiri. Waamoni walimlipa vitu hivyo katika mwaka wa pili na wa tatu pia.^e **6** Basi Yothamu akaendelea kupata nguvu, kwa maana aliziimarisha* njia zake mbele za Yehova Mungu wake.

7 Na mambo mengine katika historia ya Yothamu, vita vyake vyote na njia zake, yameandikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Israeli na wa Yuda.^f **8** Alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 16 huko Yerusalemu.^g **9** Kisha Yothamu akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.^h Na Ahazi mwanawe akawa mfalme baada yake.ⁱ

28 Ahaziⁱ alikuwa na umri wa miaka 20 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 16 huko Yerusalemu. Hakutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova kama alivyotenda Daudi babu yake.^k **2** Badala yake, alitembea katika njia za wafalme wa Israeli,^l na hata alitengeneza sanamu za chuma*^m za Mabaali. **3** Isitoshe, alifukiza moshi wa dhabihu katika Bonde la Mwana wa Hinomu* na kuwate-

27:5 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. [#]Kori moja ilikuwa sawa na lita 220 (kilogramu 170 hivi). Angalia Nyongeza B14. 27:6 *Au "alilizitayarisha." 28:2 *Au "sanamu za kuyeyushwa." 28:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Gehena."

SURA YA 27

a Yos 14:12, 13

b 2Nya 17:12

c 2Fa 9:17
2Nya 26:9, 10d Amu 11:4
2Sa 10:6
2Nya 20:1
Yer 49:1

e 2Nya 26:8

f 2Fa 15:36

g 2Fa 15:33

h 2Sa 5:9

i 2Fa 15:38

SURA YA 28

j Ho 1:1
Mik 1:1
Mt 1:9

k 2Fa 16:2

l 1Fa 12:26, 28
1Fa 16:33

m Kut 34:17

Safu ya 2

a 2Nya 33:1, 6
Yer 7:31

b Kum 12:31

c Law 26:30

d Isa 57:4, 5

e 2Fa 16:5, 6
2Nya 24:24f 2Sa 8:6
1Nya 18:5g 2Fa 15:37
Isa 7:1h 2Nya 15:2
Zb 73:27i 1Fa 16:23, 24
1Fa 22:51j Amu 2:14
Amu 3:8

keteza wanawe motoni,^a aki fuata mazoea yenye kuchukiza ya mataifa^b ambayo Yehova alikuwa ameyafukuza kutoka mbele ya Waisraeli. **4** Aliendelea pia kutoa dhabihu na kufukiza moshi wa dhabihu mahali pa juu,^c kwenye vilima, na chini ya kila mti wenye majani mengi.^d

5 Kwa hiyo Yehova Mungu wake akamtia mikononi mwa mfalme wa Siria,^e hivi kwamba wakamshinda, wakachukua mateka wengi, na kuwapeleka Damasko.^f Alitiwa pia mikononi mwa mfalme wa Israeli, ambaye aliwaua watu wake wengi. **6** Kwa maana Peka^g mwana wa Remalia aliwaua watu 120,000 huko Yuda katika siku moja, wote walikuwa wanaume jasiri, kwa sababu Waisraeli walikuwa wamemwacha Yehova Mungu wa mababu zao.^h **7** Na Zikri, shujaa Mwefraimu, alimuua Maaseya mwana wa mfalme na Azrikamu aliyekuwa msimamizi wa jumba la mfalme,* na Elkana aliyekuwa wa pili baada ya mfalme. **8** Zaidi ya hayo, Waisraeli waliwachukua mateka ndugu zao 200,000—wanawake, wana, na mabinti; walichukua pia nyara nyingi na kuzipeleka Samaria.ⁱ

9 Lakini nabii wa Yehova aliyetitwa Odedi alikuwa huko. Alienda kukutana na wanajeshi waliokuwa wakija Samaria na kuwaambia: "Tazameni! Yehova Mungu wa mababu zenu aliwatia watu wa Yuda mikononi mwenu kwa sababu walimkasirisha,^j nanyi mliwaua kwa hasira kali ambayo imefika mpaka mbinguni.

28:7 *Tnn., "nyumba."

10 Na sasa mnakusudia kuwafanya watu wa Yuda na Yerusalemu wawe watumishi wenu wa kiume na wa kike.^a Lakini, je, ninyi pia hamna hatia mbele za Yehova Mungu wenu? **11** Sasa nisikilizeni, warudisheni ndugu zenu mliowachukua mateka, kwa maana hasira ya Yehova inayowaka iko dhidi yenu.”

12 Ndipo baadhi ya wakuu wa Waefraimu, Azaria mwana wa Yehohanani, Berekia mwana wa Meshilemothi, Yehizkia mwana wa Shalumu, na Amasa mwana wa Hadlai, wakawakabili watu waliokuwa wakitoka vitani, **13** wakawaambia: “Msiwalete mateka humu, kwa maana hilo litatufanya tuwe na hatia mbele za Yehova. Mnalokusudia kufanya litaoengeza dhambi zetu na hatia yetu, kwa maana tayari tuna hatia kubwa na kuna hasira inayowaka dhidi ya Israeli.”

14 Basi wanajeshi hao wenye silaha wakawapa wakuu na kutaniko lote mateka na nyara^b walizochukua. **15** Kisha wanaume waliokuwa wamechaguliwa na kutajwa majina wakaenda na kuwachukua mateka, nao wakachukua mavazi kutoka katika zile nyara na kuwapa wote waliokuwa uchi. Basi wakawavika mavazi na kuwapa viatu, vyakula na vinywaji, na mafuta ya kujipaka. Zaidi ya hayo, waliwasafirisha kwa punda watu waliokuwa dhaifu na kuwapeleka kwa ndugu zao kule Yeriko, jiji la mitende. Kisha wakarudi Samaria.

16 Wakati huo Mfalme Ahazi aliuomba wafalme wa Ashuru wamsaidie.^c **17** Na kwa mara nyingine tena Wae-

SURA YA 28

a Law 25:39, 46
2Nya 8:9

b 2Nya 28:8

c 2Fa 16:7, 8
Isa 7:10-12

Safu ya 2

a 2Nya 26:1, 6

b 2Nya 26:10

c Yos 15:10, 12

d 2Nya 11:10

e Amu 14:1

f 2Fa 15:29
2Fa 16:7, 8
1Nya 5:26g 2Fa 17:5
Isa 7:20h 2Fa 18:15, 16
2Nya 12:9

i 2Nya 25:14

j 2Fa 16:10-13

k Yer 44:18

l 2Fa 16:17

m 1Fa 6:33, 34
2Nya 29:7

domu walivamia nchi ya Yuda, wakaishambulia na kuchukua mateka. **18** Wafilisti^a walivamia pia majiji ya Shefela^b na Negebu nchini Yuda na kuteka Beth-shemeshi,^c Aiyaloni,^d Gederothi, Soko na miji yake, Timna^e na miji yake, na Gimzo na miji yake; nao wakaanza kuishi humo. **19** Yehova aliwanyenyekeza watu wa Yuda kwa sababu ya Mfalme Ahazi wa Israeli, kwa maana aliwaacha watu wa Yuda wate nde watakavyo, na hivyo wakakosa kuwa waaminifu kwa Yehova kwa kiwango kikubwa.

20 Hatimaye Mfalme Tilgath-pilneseri^f wa Ashuru akaja kukabiliana naye na kumtesa^g badala ya kumtia nguvu. **21** Kwa maana Ahazi alikuwa amechukua kila kitu kilichokuwa katika nyumba ya Yehova na nyumba ya* mfalme^h na nyumba za wakuu na kumpa mfalme wa Ashuru kuwa zawadi; lakini hilo halikumsaidia kamwe. **22** Na wakati alipokuwa akiteseka, Mfalme Ahazi alikosa hata zaidi kuwa mwaminifu kwa Yehova. **23** Akaanza kuitolea dhabihu miungu ya Damaskoⁱ iliyokuwa imemshinda,^j akasema: “Kwa sababu miungu ya wafalme wa Siria inawasaidia, nitaitolea dhabihu ili inisaidie.”^k Lakini miungu hiyo ilimfanya yeye na Waisraeli wote wajikwae. **24** Zaidi ya hayo, Ahazi alikusanya vyombo vya nyumba ya Mungu wa kweli; akavikata vipa ndevipande vyombo vya nyumba ya Mungu wa kweli,^l akaifunga milango ya nyumba ya Yehova,^m na kujitengeneza

28:21 *Au “jumba la.”

madhabahu katika kila pembe ya Yerusalemu. **25** Na katika majiji yote ya Yuda, alijenga mahali pa juu pa kuifukizia moshi wa dhabihu miungu mingine,^a akamkasirisha Yehova Mungu wa mababu zake.

26 Na mambo mengine katika historia yake, shughuli zake zote kuanzia mwanzo mpaka mwisho, yameandikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Yuda na wa Israeli.^b **27** Kisha Ahazi akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake jijini Yerusalemu, kwa maana hawakumpeleka kwenye makaburi ya wafalme wa Israeli.^c Na Hezekia mwanawe akawa mfalme baada yake.

29 Hezekia^d alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 29 huko Yerusalemu. Mama yake alitwa Abiya binti ya Zekaria.^e **2** Aliendelea kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova,^f kama alivyofanya Daudi babu yake.^g **3** Katika mwaka wa kwanza wa utawala wake, mwezi wa kwanza, aliifungua milango ya nyumba ya Yehova na kui-rekebisha.^h **4** Kisha akawaleta makuhani na Walawi na kuwakusanya kwenye kiwanja kilichokuwa upande wa mashariki. **5** Akawaambia: “Nisikilizeni, enyi Walawi. Sasa jitakaseni na mwikakase nyumba ya Yehova Mungu wa mababu zenu, ondoeni kitu kichafu mahali patakatifu.ⁱ **6** Kwa maana baba zetu wamekosa uaminifu nao wamete nda maovu machoni pa Yehova Mungu wetu.^k Walimwacha na kugeuza nyuso zao mbali na hema la ibada la Yehova na

SURA YA 28

a 1Fa 14:22, 23
2Fa 15:32, 35
2Nya 21:5, 11
2Nya 33:1, 3

b 2Fa 16:19

c 2Nya 21:16, 20
2Nya 33:20

SURA YA 29

d Isa 1:1
Ho 1:1
Mt 1:10

e 2Fa 18:1, 2

f 2Nya 31:20

g 1Fa 15:5
2Fa 18:3

h 1Fa 6:33, 34
2Nya 28:24

i 1Nya 15:11, 12

j 2Fa 18:4

k 2Nya 28:22, 23
Yer 44:21

Safu ya 2

a Yer 2:27
Eze 8:16

b 1Fa 6:33, 34

c Law 24:2

d Kut 30:8

e Kut 29:38

f 2Nya 24:18

g Law 26:32
Kum 28:15, 25

h Law 26:14, 17

i 2Nya 28:5-8

j 2Nya 15:10-13

k Hes 3:6
Kum 10:8

l 1Nya 23:13

m Hes 4:2, 3
1Nya 23:12

n 1Nya 23:21

o 1Nya 23:7

p 1Nya 15:16, 17
1Nya 25:1, 2

q 1Nya 25:5

r 1Nya 25:1

kumgeuzia mgongo.^a **7** Pia, walifunga milango ya ukumbi^b na kuzima taa.^c Waliacha kufukiza uvumba^d na pia kumtolea Mungu wa Israeli dhabihu za kuteketezwa^e mahali patakatifu. **8** Kwa hiyo, ghadhabu ya Yehova ikaja dhidi ya watu wa Yuda na Yerusalemu,^f hivi kwamba akawafanya kuwa kitu cha kutisha na cha kushangaza na kitu cha kupigwa mluzi,^g kama mnavyoona kwa macho yenu wenyewe.^g **9** Kwa hiyo mababu zetu waliuawa kwa upanga,^h na wana wetu, mabinti wetu, na wake zetu wakapelekwa utekwani kwa sababu ya mambo hayo.ⁱ **10** Sasa ninatamani moyoni mwangu kufanya agano pamoja na Yehova Mungu wa Israeli,^j ili hasira yake inayowaka ituondokee. **11** Wanangu, huu si wakati wa kupuuzua mambo,^k kwa maana Yehova amewachagua ninyi msimame mbele zake, muwe wahudumu wake,^k na kufukiza moshi wa dhabihu zake.”^l

12 Ndipo Walawi wakasimama: Mahathi mwana wa Amasai na Yoeli mwana wa Azaria wa Wakohathi;^m kutoka kwa Wamerari,ⁿ Kishi mwana wa Abdi na Azaria mwana wa Yehaleleli; kutoka kwa Wagershoni,^o Yoa mwana wa Zima na Edeni mwana wa Yoa; **13** kutoka kwa wana wa Elisafani, Shimri na Yeueli; kutoka kwa wana wa Asafu,^p Zekaria na Matania; **14** kutoka kwa wana wa Hemani,^q Yehieli na Shimei; kutoka kwa wana wa Yeduthuni,^r Shemaya na Uzieli. **15** Kisha wakawa-

29:8 *Au “kudhihakiwa.” **29:11** *Au “kupumzika.”

kusanya pamoja ndugu zao na kujitakasa, nao wakaja kama mfalme alivyoamuru kulingana na maneno ya Yehova, ili kuitakasa nyumba ya Yehova.^a **16** Ndipo makuhani wakaingia ndani ya nyumba ya Yehova ili kuitakasa, nao wakaondoa uchafu wote uliokuwa katika hekalu la Yehova na kuupeleka kwenye ua^b wa nyumba ya Yehova. Halafu Walawi wakauchukua na kuupeleka nje katika Bonde la Kidroni.^c **17** Kwa hiyo walianza kazi hiyo ya kutakasa katika siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza, na katika siku ya nane ya mwezi huo wakafika katika ukumbi wa Yehova.^d Waliitakasa nyumba ya Yehova kwa siku nane, na katika siku ya 16 ya mwezi wa kwanza wakamaliza kazi hiyo.

18 Baada ya hayo wakaenda kwa Mfalme Hezekia na kumwambia: "Tumeitakasa nyumba yote ya Yehova, madhabahu ya dhabihu za kuteketewa^e na vyombo vyake vyote,^f na meza ya mikate ya tabaka^{*g} na vyombo vyake vyote. **19** Na vyombo vyote ambavyo Mfalme Ahazi aliviondoa wakati wa utawala wake alipokosa kutenda kwa uaminifu,^h tumevitayarisha na kuvitakasa,ⁱ navyo viko mbele ya madhabahu ya Yehova."

20 Basi Mfalme Hezekia akaamka mapema na kuwakusanya pamoja wakuu wa jiji, nao wakapanda kwenda katika nyumba ya Yehova. **21** Wakaleta ng'ombe dume saba, kondoo dume saba, wanakondoo dume saba, na mbuzi dume saba watolewe kuwa dhabihu

SURA YA 29

a 2Nya 29:5

b 1Fa 6:36

c 2Fa 23:4, 6
2Nya 15:16
Yoh 18:1d 1Fa 6:3
1Nya 28:11

e 2Nya 4:1

f 1Fa 7:40

g 1Fa 7:48

h 2Nya 28:1, 2
2Nya 28:24

i 2Nya 29:5

Safu ya 2

a Law 4:3
Law 4:13, 14
Hes 15:22-24

b Law 4:4

c Law 4:7, 18

d 1Nya 25:1, 6
2Nya 9:11e 1Nya 28:12, 13
2Nya 8:12, 14f 2Sa 24:11, 12
1Nya 29:29g 2Sa 7:2
2Sa 12:1h Hes 10:8
1Nya 15:24

i Law 1:3, 4

ya dhambi kwa ajili ya ufalme, kwa ajili ya mahali patakatifu, na kwa ajili ya watu wa Yuda.^a Basi akawaambia makuhani, wazao wa Haruni, wawatoe dhabihu kwenye madhabahu ya Yehova. **22** Kisha wakawachinja ng'ombe hao,^b na makuhani wakachukua damu yao na kunyunyiza kwenye madhabahu;^c halafu wakawachinja wale kondoo dume na kunyunyiza damu yao kwenye madhabahu, kisha wakawachinja wanakondoo dume hao na kunyunyiza damu yao kwenye madhabahu. **23** Kisha wakawaleta wale mbuzi dume wa dhabihu ya dhambi mbele ya mfalme na kutaniko na kuweka mikonono yao juu yao. **24** Makuhani wakawachinja na kutoa dhabihu ya dhambi kwenye madhabahu wakitumia damu yao, ili kufunika dhambi za Waisraeli wote, kwa sababu mfalme alisema kwamba dhabihu ya kuteketewa na dhambi hu ya dhambi ilipaswa kutolewa kwa ajili ya Waisraeli wote.

25 Wakati huo, aliwaweka Walawi katika nyumba ya Yehova wakiwa na matoazi, vinanda, na vinubi,^d kulingana na amri ya Daudi^e na ya Gadi^f mwonaji wa mfalme na ya nabii Nathani,^g kwa maana amri hiyo ilitoka kwa Yehova kupitia manabii wake. **26** Basi Walawi walikuwa wakisimama wakiwa na ala za Daudi, na makuhani wakiwa na tarumbeta.^h

27 Kisha Hezekia akaagiza dhabihu ya kuteketewa itolewe kwenye madhabahu.ⁱ Dhabihu ya kuteketewa ilipoanza kutolewa, wimbo wa Yehova ulianza na pia milio ya

tarumbeta, kwa kufuata mwingozi wa ala za Mfalme Daudi wa Israeli. **28** Na kutaniko lote likainama chini wimbo huo ulipokuwa ukiimbwa na tarumbeta kupigwa—yote hayo yaliendelea mpaka walipomaliza kutoa dhabihu ya kuteketezwa. **29** Na mara tu walipomaliza kutoa dhabihu hiyo, mfalme na wote walio-kuwa pamoja naye wakainama chini na kusujudu. **30** Sasa Mfalme Hezekia na wakuu wakawaambia Walawi wamsifu Yehova kwa maneno ya Daudi^a na ya mwonaji Asafu.^b Kwa hiyo wakamsifu kwa shangwe nyingi, nao wakainama chini na kusujudu.

31 Kisha Hezekia akasema: “Sasa kwa kuwa mmetengwa kando* kwa ajili ya Yehova, njooni mlete dhabihu mbalimbali na dhabihu za shukrani katika nyumba ya Yehova.” Basi kutaniko likaanza kuleta dhabihu mbalimbali na dhabihu za shukrani, na kila mtu aliyekuwa na moyo wa kutoa kwa hiari alileta dhabihu za kuteketezwa.^c **32** Idadi ya dhabihu za kuteketezwa zilizoletwa na kutaniko ilikuwa ng’ombe 70, kondoo dume 100, wanakondoo dume 200—wote hao wakiwa dhabihu ya kuteketezwa kwa Yehova^d—**33** na dhabihu takatifu zilikuwa ng’ombe 600 na kondoo 3,000. **34** Lakini hakukuwa na makuhani wa kutosha kuwachuna ngozi wanyama wote wa dhabihu za kuteketezwa, kwa hiyo ndugu zao Walawi waliwasaidia^e mpaka kazi hiyo ilipoisha na mpaka makuhani

29:31 *Tnn., “Sasa mmeujaza mkono wenu.”

SURA YA 29

a 2Sa 23:1

b 1Nya 16:7

c Law 1:3

d 1Fa 3:4
1Fa 8:63
1Nya 29:21, 22e Hes 8:19
2Nya 30:17
2Nya 35:10, 11

Safu ya 2

a 2Nya 30:2, 3

b 2Nya 29:32

c Law 3:1
Law 3:14-16

d Hes 15:5

e 2Nya 30:12

SURA YA 30

f 2Nya 11:14, 16

g 2Nya 34:1, 6, 7

h Kut 12:43
Law 23:5
Kum 16:2
2Nya 35:1

i Hes 9:10, 11

j Kut 12:18

k 2Nya 29:34

l Amu 18:29

walipoweza kujitakasa,^a kwa kuwa Walawi walikuwa na bidii zaidi ya* kujitakasa kuliko makuhani. **35** Pia, kulikuwa na dhabihu nyingi za kuteketezwa,^b na vilevile vipande vya mafuta vya dhabihu za ushirika^c na matoleo ya vinywaji kwa ajili ya dhabihu za kuteketezwa.^d Hivyo utumishi wa nyumba ya Yehova ukaa-nzishwa tena.* **36** Kwa hiyo Hezekia na watu wote wakashangilia jambo ambalo Mungu wa kweli alikuwa amewafanya watu,^e kwa sababu jambo hilo lilitendeka haraka sana.*

30 Hezekia akatuma ujumbe kwa watu wote wa Israeli^f na Yuda, na hata aliwaandikia barua watu wa Efraimu na Manase^g waje Yerusalemu katika nyumba ya Yehova kuadhimisha Pasaka ya Yehova Mungu wa Israeli.^h **2** Hata hivyo, mfalme, wakuu wake, na kutaniko lote Yerusalemu likaaamua kuadhimisha Pasaka katika mwezi wa pili,ⁱ **3** kwa maana hawakuweza kuiadhimisha wakati ambapo iliadhimishwa kwa ukawaida,^j kwa sababu haku-kuwa na makuhani wa kutosha waliojitakasa^k na watu hawakuwa wamekusanyika Yerusalemu. **4** Mpango huo ulionekana kuwa mzuri machoni pa mfalme na kutaniko lote. **5** Basi wakaamua kutangaza kotekote Israeli, kuanzia Beersheba mpaka Dani,^l kwamba watu waje Yerusalemu kuadhimisha Pasaka ya Yehova Mungu wa Israeli, kwa maa-

29:34 *Tnn., “walikuwa na moyo mnyoofu katika.” 29:35 *Au “ukatayarishwa.” 29:36 *Au “ghafila.”

na wakiwa kikundi hawakuwa wameiadhimisha kulingana na yaliyoandikwa.^a

6 Kisha wajumbe* wakanda kotekote Israeli na Yuda wakiwa na barua hizo kutoka kwa mfalme na wakuu wake, kama mfalme alivyoamuru, akisema: “Watu wa Israeli, rudini kwa Yehova Mungu wa Abrahamu, Isaka, na Israeli, ili naye arudi kwa watu waliobaki walioponyoka kutoka mikononi mwa wafalme wa Ashuru.^b **7** Msiwe kama mababu zenu na kama ndugu zenu waliokosa kutenda kwa uaminifu kwa Yehova Mungu wa mababu zao, hivi kwamba akawafanya kuwa kitu cha kutisha, kama mnavyoona.^c **8** Sasa msiwe wakaidi kama mababu zenu.^d Jinyenyekezeni kwa Yehova, nanyi mje mahali pake patakatifu^e ambapo amepataka milele, mumtumikie Yehova Mungu wenu, ili hasira yake inayowaka iwao ndokee.^f **9** Kwa maana mkirudi kwa Yehova, ndugu zenu na wana wenu wataonyesha rehema na wale waliowateka,^g nao wataruhusiwa kurudi katika nchi hii;^h kwa maana Yehova Mungu wenu ni mwenye huruma* na rehema,ⁱ naye hataugeza uso wake mbali nanyi mkirudi kwake.”^j

10 Kwa hiyo wajumbe* hao walienda jiji hadi jiji katika nchi yote ya Efraimu na Manase,^k walifika hata Zabuloni, lakini watu walikuwa wakiwafanyia mzaha na kuwadhihaki.^l **11** Hata hivyo, watu fulani kutoka Asheri, Manase, na Zabuloni walijinyenyekeza na

30:6, 10 *Tnn., “wakimbiaji.” 30:9 *Au “neema.”

SURA YA 30

a 2Nya 35:18

b 2Fa 15:29
1Nya 5:26
2Nya 28:20, 21

c 2Nya 29:8, 9

d Kut 32:9

e Kum 12:5, 6
Zb 132:13

f 2Nya 29:10

g 1Fa 8:49, 50

h Kum 30:1-3

i Kut 34:6
Zb 86:5
Mik 7:18j 2Nya 15:2
Isa 55:7
Yak 4:8

k 2Nya 30:1

l 2Nya 36:15, 16

Safu ya 2

a 2Nya 11:14, 16

b Hes 9:10, 11

c Law 23:6

d 2Fa 18:22

e 2Nya 28:24

f Law 1:5

g 2Nya 29:34

h 2Nya 30:1

i Zb 86:5

kuja Yerusalemu.^a **12** Mko-no wa Mungu wa kweli ulikuwa pia juu ya watu wa Yuda ili kuwaunganisha* watekeleze yale ambayo mfalme na wakuu walikuwa wameamuru kulingana na neno la Yehova.

13 Umati wa watu ulikusanyika Yerusalemu katika mwezi wa pili^b kuadhimisha She-rehe ya Mikate Isiyo na Chachu;^c lilikuwa kutaniko kubwa sana. **14** Basi wakaondoa madhabahu zilizokuwa Yerusalemu,^d wakaziondoa madhabahu zote za kufukizia uvumba^e na kuzitupa katika Bonde la Kidroni. **15** Kisha wakamchinja mnyama wa Pasaka katika siku ya 14 ya mwezi wa pili. Makuhani na Walawi wakaona aibu, kwa hiyo wakajitakasa na kuleta dhabihu za kuteketezwa katika nyumba ya Yehova. **16** Nao wakasimama katika nafasi zao za kawaida, kulingana na Sheria ya Musa, mtu wa Mungu wa kweli; kisha makuhani wakanyunyiza damu^f waliyokabidhiwa na Walawi. **17** Kulikuwa na watu wengi katika kutaniko hilo ambao hawakuwa wamejitakasa, na Walawi ndio waliowachinja wanyama wa dhabihu za Pasaka kwa ajili ya wote ambao hawakuwa safi,^g ili wawatakase kwa Yehova. **18** Kwa maana idadi kubwa ya watu, hasa wale waliotoka Efraimu, Manase,^h Isakari, na Zabuloni, hawakuwa wamejitakasa, lakini bado walikula Pasaka, kinyume cha mambo yaliyoandikwa. Lakini Hezekia alisali kwa ajili yao, akisema: “Yehova, wewe uliye mweni,ⁱ msamehe **19** kila mtu

30:12 *Tnn., “kuwapa moyo mmoja.”

ambaye ameutayarisha moyo wake ili kukutafuta wewe Mungu wa kweli,^a Yehova, Mungu wa mababu zake, ingawa hatakaswa kulingana na kiwango cha utakatifu.”^b **20** Basi Yehova akamsikiliza Hezekia, akawasamehe* watu hao.

21 Kwa hiyo Waisraeli walio kuwa Yerusalemu wakaadhimisha Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu^c kwa siku saba, wakiva na shangwe nyingi,^d na Walawi na makuhani walikuwa wakimsifu Yehova siku baada ya siku, wakimpigia Yehova ala zao kwa sauti kubwa.^e

22 Zaidi ya hayo, Hezekia alizungumza na Walawi wote waliokuwa wakimtumikia Yehova kwa busara, akawatia moyo.* Nao wakala katika kipindi chote cha sherehe hiyo ya siku saba,^f wakitoa dhabihu za ushirika^g na kumshukuru Yehova Mungu wa mababu zao.

23 Kisha kutaniko lote likaamua kuendelea na sherehe hiyo kwa siku saba zaidi, kwa hiyo waliifanya kwa siku saba zaidi huku wakishangilia.^h **24** Na Mfalme Hezekia wa Yuda alitoa mchango wa ng’ombe dume 1,000 na kondoo 7,000 kwa ajili ya kutaniko, na wakuu walitoa mchango wa ng’ombe dume 1,000 na kondoo 10,000 kwa ajili ya kutaniko;ⁱ na makuhani wengi walikuwa wakijitakasa.^j **25** Na kutaniko lote la Yuda, makuhani, Walawi, kutaniko lote lililotoka Israeli,^k na wakaaji wageni^l waliotoka katika nchi ya Israeli na wale walioishi Yuda wakaendelea kushangilia. **26** Na kulikuwa na

30:20 *Tnn., “akawaponya.” 30:22 *Tnn., “akazungumza na moyo wao.”

SURA YA 30

a 2Nya 19:2, 3
Ezr 7:10

b Hes 9:6, 10

c Law 23:6

d Kum 12:5, 7
Ne 8:10

e 2Nya 29:25

f Law 23:6

g Law 3:1

h 1Fa 8:65

i 2Nya 35:7, 8

j 2Nya 29:34

k 2Nya 30:11, 18

l Kut 12:49

Safu ya 2

a 1Fa 8:65, 66

b Hes 6:23-26
Kum 10:8

SURA YA 31

c Kut 23:24

d Kum 7:5
2Fa 18:1, 4
2Nya 14:2, 3
2Nya 34:1, 3

e Kum 12:2

f 2Nya 23:16, 17

g 2Nya 30:1, 18

h 1Nya 24:1

i 1Nya 23:6

j 2Nya 8:14

k 1Nya 23:13
1Nya 23:27-30

l 2Nya 30:24

m Kut 29:39

n Hes 28:9

o Hes 10:10

p Kum 16:16

shangwe nyingi Yerusalemu, kwa maana tangu siku za Sulamani mwana wa Daudi mfalme wa Israeli, jambo kama hilo halikuwa limeonekana Yerusalemu.^a **27** Hatimaye makuhani Walawi wakasimama na kuwabariki watu;^b na Mungu akasikia sauti yao, na sala yao ikafika katika makao yake matakatifu, mbinguni.

31 Mara tu walipomaliza kufanya mambo hayo yote, Waisraeli wote waliokuwepo wakaenda katika majiji ya Yuda, nao wakazivunjavunja nguzo takatifu,^c wakaikatakata miti mitakatifu,^d na kubomoa mahali pa juu^e na madhabahu^f katika nchi yote ya Yuda na Benjamini, na pia kule Efraimu na Manase,^g mpaka walipoviharibu kabisa vitu hivyo, kisha Waisraeli wote wakarudi katika majiji yao, kila mmoja kwenye miliki yake.

2 Kisha Hezekia akawaweka makuhani katika vikundi vyao^h na Walawi katika vikundi vyao,ⁱ kila kuhani na Mlawi katika utumishi wake,^j kwa ajili ya dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za ushirika, ili wahudumu na kushukuru na kusifu katika malango ya nyua* za Yehova.^k **3** Baadhi ya mali za mfalme mwenyewe zilitolewa kwa ajili ya dhabihu za kuteketezwa,^l kutia ndani dhabihu zilizotolewa asubuhi na jioni,^m na pia dhabihu za kuteketezwa kwa ajili ya Sabato,ⁿ miezi mipya,^o na sherehe mbalimbali,^p kulingana na mambo yaliyoandikwa katika Sheria ya Yehova.

31:1 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 31:2 *Tnn., “kambi.”

4 Isitoshe, aliwaamuru watu walioishi Yerusalemu watoe fungu ambalo makuhani na Walawi walistahili kupokea,^a ili waishike kabisa* sheria ya Yehova. 5 Mara tu agizo hilo lilipotolewa, Waisraeli walitoa kwa wingi mazao ya kwanza ya nafaka, divai mpya, mafuta,^b na asali, na mazao yote ya shambani;^c walileta kwa wingi sehemu ya kumi ya kila kitu.^d 6 Na watu wa Israeli na wa Yuda waliokuwa wakiishi katika majiji ya Yuda walileta pia sehemu ya kumi ya ng'ombe na kondoo na sehemu ya kumi ya vitu vitakatifu^e vilivyotakaswa kwa ajili ya Yehova Mungu wao. Walivileta na kuvipanga katika marundo mengi. 7 Katika mwezi wa tatu,^f walianza kuvipanga katika marundo vitu walivyotoa michango; na katika mwezi wa saba^g wakamaliza. 8 Hezekia na wakuu walipokuja na kuona marundo hayo, walimsifu Yehova na kuwabariki watu wake Waisraeli.

9 Hezekia akawauliza makuhani na Walawi kuhusu marundo hayo, 10 ndipo Azaria mkuu wa makuhani wa nyumba ya Sadoki akamwambia: "Tangu watu walipoanza kuleta michango ndani ya nyumba ya Yehova,^h wamekuwa wakila na kushiba na bado kiasi kikubwa kimebaki, kwa maana Yehova amewabariki watu wake, na kiasi hiki kikubwa sana kimebaki."ⁱ

11 Ndipo Hezekia akawaambia watawarishe vyumba vya kuhifadhia vitu hivyo^{*j} katika nyumba ya Yehova, basi wakavitayarisha. 12 Waliende-

31:4 *Au "wajitoe kikamili kwa." 31:11 *Au "vyumba vya kulia chakula."

SURA YA 31

a Hes 18:21
Ne 10:38, 39

b Hes 18:12

c Kut 22:29
Kut 23:19
Ne 10:37

d Met 3:9

e Law 27:30
Kum 14:28

f Law 23:16

g Law 23:24

h Hes 18:8

i Mal 3:10

j Ne 10:38, 39
Ne 12:44

Safu ya 2

a Law 27:30
Kum 14:28

b 1Nya 26:17,19

c Kum 12:5, 6
Kum 16:10

d Hes 18:8

e Law 2:10
Law 7:1

f Yos 21:19

g 1Nya 24:1

h 1Nya 24:4

i Hes 4:2, 3
Hes 8:24
1Nya 23:24

j 1Nya 23:6

lea kuleta kwa uaminifu michango, sehemu za kumi,^a na vitu vitakatifu; na Mlawi aliyeitwa Konania aliwekwa kuwa msimamizi wa vitu hivyo vyote, na Shimei ndugu yake alikuwa wa pili. 13 Yehieli, Azazia, Nahathi, Asaheli, Yerimothi, Yozabadi, Elieli, Ismakia, Mahathi, na Benaya walikuwa maofisa waliomsaidia Konania na Shimei ndugu yake, kama Mfalme Hezekia alivyoagiza, na Azaria alikuwa msimamizi wa nyumba ya Mungu wa kweli. 14 Na Kore mwana wa Imna, Mlawi aliye kuwa mlinzi wa malango upande wa mashariki,^b alisimamia matoleo ya hiari^c ya Mungu wa kweli, naye aligawa mchango uliotolewa kwa Yehova^d na pia vitu vitakatifu kabisa.^e 15 Na Edeni, Miniadini, Yeshua, Shemaya, Amaria, na Shekania walikuwa chini ya usimamizi wake katika majiji ya makuhani,^f katika wadhifa wao wa kuaminiwa, ili wawagawie ndugu zao kwa usa wa katika vikundi,^g wakubwa kwa wadogo. 16 Hilo halikutia ndani mchango waliogawiwa wanaume wenye umri wa miaka mitatu na zaidi walioandikishwa kwenye orodha ya koo, ambao walikuja kila siku kutumikia katika nyumba ya Yehova na kutimiza majukumu ya vikundi vyao.

17 Makuhani waliandikishwa katika orodha ya koo kulingana na ukoo wao,^{*h} kama walivyoandikishwa Walawi waliokuwa na umri wa miaka 20 na zaidi,ⁱ kulingana na majukumu ya vikundi vyao.^j 18 Walioandikishwa

31:17 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

katika orodha ya koo wali-tia ndani watoto wao wote, wake zao, wana wao, na mabinti wao, kutaniko lote—kwa maana walidumisha utakaso wao kwa ajili ya mambo matakatifu kwa sababu ya wadhifa wao wa kuaminiwa— **19** na pia wazao wa Haruni, maku-hani walioishi katika mashamba yenye malisho ambayo yalizunguka majiji yao.^a Katika majiji yote, wanaume walikuwa wamechaguliwa na kutajwa majina ili wampe mafungu kila mwanamume kuhani na kila mtu aliyeandikishwa katika orodha ya koo za Walawi.

20 Hezekia alifanya hayo katika nchi yote ya Yuda, naye aliendelea kutenda mema na yaliyo sawa na ya uaminifu mbele za Yehova Mungu wake. **21** Na kila kazi aliyofanya ili kumtafuta Mungu wake, iwe ni kuhusiana na utumishi wa nyumba ya Mungu wa kweli^b au kuhusiana na Sheria na amri, alifanya kwa moyo wote, naye alifanikiwa.

32 Baada ya mambo hayo na matendo hayo ya uaminifu,^c Mfalme Senakeribu wa Ashuru alikuja na kuvamia Yuda. Alizingira majiji yenye ngome, akikusudia kuvunja na kuingia ndani na kuyateka.^d

2 Hezekia alipoona kwa mba Senakeribu amekuja akikusudia kulishambulia jiji la Yerusalemu, **3** alishauriana na wakuu wake na mashujaa wake na kuamua kuziba chemchemi za maji zilizokuwa nje ya jiji,^e nao wakamsaidia. **4** Watu wengi walikusanywa, nao wakaziba chemchemi zote na kijito kilichopita nchini, wakisema: “Kwa nini wafal-

SURA YA 31

a Law 25:33, 34
Hes 35:2
Yos 21:13

b 2Nya 29:35

SURA YA 32

c 2Nya 31:20

d 2Fa 18:7,13
Isa 36:1

e 2Fa 20:20

Safu ya 2

a 2Sa 5:9
1Fa 9:24
1Fa 11:27
2Fa 12:20

b 2Fa 19:6

c Kum 31:6, 8
Yos 1:6, 9
2Fa 6:16, 17
2Nya 20:15

d Hes 14:9
Kum 20:1, 4
Yos 10:42
Yer 17:5

e 2Nya 20:20

f Isa 37:8

g 2Fa 18:17
Isa 36:2

h 2Fa 18:19
Isa 36:4

me wa Ashuru waje na kupata maji mengi?”

5 Zaidi ya hayo, akiwa amezimia, alijenga upya ukuta wote uliobomolewa, akajenga minara juu yake, na kujenga ukuta mwingine upande wa nje. Alirekebisha pia Kilima^{*a} cha Jiji la Daudi na kutengeneza silaha nyingi na ngao. **6** Kisha akawachagua wakuu wa majeshi wawaongoze watu, akawakusanya kwenye uwanja wa jiji uliokuwa karibu na lango la jiji, akawatia moyo^{*} akisema: **7** “Iweni jasiri na imara. Msio-gope wala msihofu kwa sababu ya mfalme wa Ashuru^b na umati wote ulio pamoja naye, kwa maana walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja naye.^c **8** Yeye anategemea mkono wa nyama^{*} lakini sisi tuna Yehova Mungu wetu wa kutusaidia na kupigana vita vyetu.”^d Basi watu wakaimarishwa na maneno ya Mfalme Hezekia wa Yuda.^e

9 Baada ya hayo, Mfalme Senakeribu wa Ashuru alipo-kuwa Lakishi^f pamoja na fahari yake yote ya kifalme,^{*} aliwatuma watumishi wake Yerusalemu, kwa Mfalme Hezekia wa Yuda na kwa Wayudea wote waliokuwa Yerusalemu,^g akisema:

10 “Mfalme Senakeribu wa Ashuru anasema hivi: ‘Ni nini mnachotumainia kinachowafanya mkae Yerusalemu wakati limezingirwa?’^h **11** Je, Hezekia hawapotoshi ili mfe kwa njaa kali na kiu, anapose-

32:5 *Au “Milo.” Neno la Kiebrania linalomaanisha “jaza.” **32:6** *Tnn., “akazungumza na moyo wao.” **32:8** *Au “nguvu za mwanadamu.” **32:9** *Au “uwezo wake wote wa kijeshi na fahari.”

ma: "Yehova Mungu wetu atatuokoa kutoka mikononi mwa mfalme wa Ashuru?"^a **12** Je, siye Hezekia huyuhuyu aliyeondoa mahali pa juu^b pa Mungu wenu na madhabahu Zake^c kisha akawaambia watu wa Yuda na Yerusalemu: "Mnapaswa kuinama mbele ya madhabahu moja na kufukiza moshi wa dhabihu zenu?"^d **13** Je, hamjui yale ambayo mimi na mababu zangu tuliyatendea mataifa yote ya nchi mbalimbali?^e Je, miungu ya mataifa ya nchi hizo iliweza kuwaokoa kutoka mikononi mwangu?^f **14** Ni mungu gani kati ya miungu yote ya mataifa hayo ambayo mababu zangu waliiangamiza aliyeweza kuwaokoa watu wake kutoka mikononi mwangu, hivi kwamba Mungu wenu aweze kuwaokoa ninyi kutoka mikononi mwangu?^g **15** Sasa msiache Hezekia awadanganye au kuwapotosha hivyo!^h Msimwamini, kwa maana hakuna mungu yeyote wa taifa lolote au ufalme aliyeweza kuwaokoa watu wake kutoka mikononi mwangu na kutoka mikononi mwa mababu zangu. Basi, Mungu wenu atawezaje kuwaokoa ninyi kutoka mikononi mwangu?"ⁱ

16 Watumishi wake wakasema mambo mengi zaidi mabaya dhidi ya Yehova Mungu wa kweli na dhidi ya Hezekia mtumishi wake. **17** Aliandika pia barua^j za kumtukana Yehova Mungu wa Israeli^k na kusema mambo mabaya dhidi yake, akisema: "Kama miungu ya mataifa ya nchi mbalimbali ilivyoshindwa kuwaokoa watu wake kutoka mikononi mwangu,^l vivyo hivyo Mungu

SURA YA 32

a 2Fa 18:29, 30
2Fa 19:10

b 2Fa 18:1, 4

c 2Nya 31:1

d 2Fa 18:22
Isa 36:7e 2Fa 15:29
2Fa 17:5
Isa 37:12f 2Fa 18:33, 34
2Fa 19:17, 18g Kut 14:3
Kut 15:9

h 2Fa 18:29

i Kut 5:2
Kum 32:27
Da 3:14, 15

j 2Fa 19:14

k Isa 37:29

l 2Fa 17:6
2Fa 19:12

Safu ya 2

a 2Fa 18:26, 28
Isa 36:11, 13b 2Fa 19:2, 20
Isa 37:2c 2Fa 19:14, 15
2Nya 14:11

d Zb 76:5

e 2Fa 19:35-37
Isa 37:37, 38f 1Fa 4:21
2Nya 17:1, 5g 2Fa 20:1, 2
Isa 38:1, 2h 2Fa 20:5, 9
2Nya 32:31
Isa 38:8

wa Hezekia hatawaokoa watu wake kutoka mikononi mwangu." **18** Waliendelea kuwaambia watu wa Yerusalemu waliokuwa ukutani mambo hayo kwa sauti kubwa kwa lugha ya Wayahudi, ili wawaogopeshe na kuwatia hofu, na ili waliteke jiji.^a **19** Walisema mambo mabaya dhidi ya Mungu wa Yerusalemu kama walivyosema dhidi ya miungu ya mataifa yaliyo duniani, ambayo ni kazi ya mikono ya mwanadamu. **20** Lakini Mfalme Hezekia na nabii Isaya^b mwana wa Amози waliendelea kusali kuhusu jambo hilo na kuzililia mbingu ili wapate msaada.^c

21 Ndipo Yehova akamtuuma malaika, na malaika huyo akamwagamiza kabisa kila shujaa hodari,^d kiongozi, na mkuu katika kambi ya mfalme wa Ashuru, hivi kwamba akarudi katika nchi yake akiwa ameabika. Baadaye alilingia katika nyumba ya* mungu wake, na humo baadhi ya wanawe mwenyewe waka muua kwa upanga.^e **22** Basi Yehova akamwokoia Hezekia na wakaaji wa Yerusalemu kutoka mikononi mwa Mfalme Senakeribu wa Ashuru na kutoka mikononi mwa wengine wote na kuwapumzisha pande zote. **23** Na watu wengi wakamletea Yehova zawadi huko Yerusalemu na kumletea Mfalme Hezekia wa Yuda vitu bora,^f naye akaheshimiwa sana na mataifa yote baada ya mambo hayo.

24 Siku hizo Hezekia akawa mgonjwa karibu afe, akasali kwa Yehova,^g naye akamjibu na kumpa ishara.^{*h}

32:21 *Au "hekalu la." 32:24 *Au "kumfanyia muujiza."

25 Lakini Hezekia hakuonyesha uthamini kwa wema wote aliotendewa, kwa maana moyo wake uliingiwa na kiburi, jambo lililomfanya yeye pamoja na watu wa Yuda na wa Yerusalemu wapatwe na ghadhabu. **26** Hata hivyo, Hezekia alijinyenyekeza, moyo wake ukaacha kuwa na kiburi,^a yeye pamoja na wakaaji wa Yerusalemu, na ghadhabu ya Yehova haikuja dhidi yao katika siku za Hezekia.^b

27 Hezekia akapata utajiri mwingi sana na utukufu;^c akajijengea maghala^d ya kuweka fedha, dhahabu, mawe yenye thamani, mafuta ya zeri, ngao, na vitu vyote vyenye kutamani. **28** Alijenga pia maghala ya mazao ya nafaka na divai mpya na mafuta, na pia mabandaa kwa ajili ya mifugo ya kila aina na mabanda kwa ajili ya kondoo na mbuzi. **29** Pia alijijengea majiji, akapata mifugo mingi sana, makundi ya kondoo, mbuzi, na ng'ombe, kwa maana Mungu alimpa mali nyingi sana. **30** Hezekia ndiye aliyeziba chemchemi ya juu ya maji^e ya Gihoni^f na kuyaelekeza moja kwa moja chini upande wa magharibi katika Jiji la Daudi,^g na Hezekia alifanikiwa katika kila kazi aliyofanya. **31** Hata hivyo, wasemaji wa wakuu wa Babiloni walipotumwa wamuulize kuhusu ishara^h iliyokuwa imetokea* nchini,ⁱ Mungu wa kweli alimwacha ili kumjaribu,^j ili ajue mambo yote yaliyokuwa moyoni mwake.^k

32 Na mambo mengine katika historia ya Hezekia na matendo yake ya upendo mshika-

32:31 *Au “muujiza uliokuwa ume-tokea.”

SURA YA 32

a Yer 26:18, 19

b 2Fa 20:19

c 2Nya 1:11, 12
2Nya 17:1, 5

d 1Fa 9:17-19

e 2Nya 32:4

f 1Fa 1:33, 45

g 2Sa 5:9

h 2Fa 20:8-11
Isa 38:8i 2Fa 20:12
Isa 39:1

j Mwa 22:1

k Kum 8:2
Zb 7:9
Zb 139:23

Safu ya 2

a 2Nya 31:20, 21

b Isa 1:1

c 2Fa 20:20

d 1Fa 11:43

SURA YA 33

e Mt 1:10

f 2Fa 21:1

g 2Fa 21:2-6

h 2Fa 18:1, 4

i Kum 4:19
2Fa 23:5

j 2Fa 16:10, 11

k Kum 12:11
2Nya 6:6l 1Fa 6:36
1Fa 7:12

m 2Fa 16:1, 3

n Yos 15:8, 12
2Fa 23:10

o Law 19:26

p Law 20:6
Kum 18:10, 11

manifu,^a yameandikwa katika maono ya nabii Isaya,^b mwana wa Amози, katika Kitabu cha Wafalme wa Yuda na wa Israeli.^c **33** Kisha Hezekia akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake kwenye njia inayopanda kuelekea kwenye makaburi ya wana wa Daudi;^d na watu wote wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu wakamheshimu alipokufa. Na Manase mwana-
we akawa mfalme baada yake.

33 Manase^e alikuwa na umri wa miaka 12 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 55 huko Yerusalemu.^f

2 Alitenda maovu machoni pa Yehova, akafuata mazoea yenye kuchukiza ya mataifa ambayo Yehova alikuwa ameyafukuza kutoka mbele ya Waisraeli.^g **3** Alijenga upya mahali pa juu ambapo Hezekia baba yake alikuwa amebomoa,^h akajenga madhabahu kwa ajili ya Mabaali na kutengeneza miti mitakatifu,ⁱ naye akaliinamia jeshi lote la mbinguni na kuliabudu.^j **4** Alijenga pia madhabahu katika nyumba ya Yehova,^j ambayo Yehova alikuwa amesema hivi kuihusu: “Nitaweka jina langu Yerusalemu milele.”^k **5** Naye alijenga madhabahu kwa ajili ya jeshi lote la mbinguni katika nyuma mbili za nyumba ya Yehova.^l **6** Na pia aliwateketeza* motoni wanawe mwenyewe^m katika Bonde la Mwana wa Hinomu;ⁿ alifanya uchawi,^o alifanya uaguzi,[#] alifanya ulozu, na kuwaweka rasmi watu wanaowasiliana na roho na wabashiri.^p Alitenda kwa kiwango kiku-

33:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 33:6 *Tnn., “aliwapitisha.” #Au “alibashiri.”

bwa sana mambo maovu machoni pa Yehova, na kumkasi-risha.

7 Sanamu aliyokuwa amechonga aliweka katika nyumba ya Mungu wa kweli^a ambayo Mungu alikuwa amewambia hivi Daudi na Sulemani mwanawe kuihusu: "Nitaweka jina langu milele katika nyumba hii na katika jiji la Yerusalemu, ambalo nimelichagua kati ya makabila yote ya Israeli.^b **8** Ikiwa Waisraeli watashika kwa uangalifu mambo yote niliyowaa-muru, Sheria yote, masharti na amri nilizowapa* kupitia Musa mtumishi wangu, sitaiondoa tena kamwe miguu yao katika nchi niliyowapa mababu zao." **9** Manase aliendelea kuwapotosha watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu, akasababisha watende mambo maovu zaidi kuliko mataifa ambayo Yehova alikuwa ameyaangamiza kutoka mbele ya Waisraeli.^c

10 Yehova aliendelea kuzungumza na Manase na watu wake, lakini hawakumsikiliza.^d **11** Kwa hiyo Yehova akawaleta wakuu wa jeshi la mfalme wa Ashuru ili wawashambulie, nao wakamkamata Manase kwa kulabu* na kumfunga kwa pingu mbili za shaba na kumpeleka Babiloni. **12** Alipokuwa akite-seka, alimsihi* Yehova Mungu wake amwonyeshe kibali, naye akaendelea kujinyenye-keza sana mbele za Mungu wa mababu zake. **13** Aliendelea kusali kwa Mungu, naye aka-

33:8 *Tnn., "maamuzi ya hukumu niliyowapa." **33:11** *Au labda, "mashimoni." **33:12** *Au "aliutuliza uso wa Yehova Mungu wake."

SURA YA 33

a 2Fa 23:6

b 2Fa 21:7-9
2Fa 23:27
2Nya 7:16

c Law 18:24
Yos 24:8
2Fa 21:11, 16

d 2Nya 36:15, 16

Safu ya 2

a Isa 1:18

b Da 4:25

c 2Sa 5:9
2Nya 32:2, 5

d 2Nya 32:30

e Ne 3:3

f 2Nya 27:1, 3

g 2Fa 21:1, 7

h 2Fa 21:1, 4, 5

i 2Nya 29:18

j Law 3:1

k Law 7:12

l 2Nya 33:12, 13

m 2Fa 21:2, 9

n 2Fa 21:3, 7

guswa na sala yake ya kusihi, akasikia ombi lake la kutaka kibali, akamrudisha Yerusalemu kwenye ufalme wake.^a Ndi-po Manase akajua kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli.^b

14 Baada ya hayo alijenga ukuta wa nje wa Jiji la Daudi^c upande wa magharibi wa Gihoni,^d bondeni,^e na mpaka kwenye Lango la Samaki,^e akauzungusha hadi Ofeli,^f na kuu-fanya uwe mrefu sana. Zaidi ya hayo, aliwaweka wakuu wa jeshi katika majiji yote yenye ngome nchini Yuda. **15** Kisha akaondoa katika nyumba ya Yehova^g miungu wa kigeni na ile sanamu iliyochongwa na pia madhabahu zote alizokuwa amejenga kwenye mlima wa nyumba ya Yehova^h na Yerusalemu, akaagiza vitu hivyo vitupwe nje ya jiji. **16** Aliitayarisha pia madhabahu ya Yehova,ⁱ akaanza kutoa juu yake dhabihu za ushirika^j na dhabihu za shukrani,^k naye akawambia watu wa Yuda wamtumiekie Yehova Mungu wa Israeli. **17** Hata hivyo, bado watu walikuwa wakitoa dhabihu mahali pa juu, ila tu sasa walimtolea Yehova Mungu wao.

18 Na mambo mengine katika historia ya Manase, sala aliyotoa kwa Mungu wake, na maneno ya waonaji waliozungumza naye katika jina la Yehova Mungu wa Israeli, yameandikwa katika historia ya wafalme wa Israeli. **19** Pia sala yake^l na jinsi ombi lake lilivyojibiwa, dhambi zake zote na jinsi alivyokosa kuwa mwaminifu,^m sehemu alizojenga mahali pa juu na kusimamisha miti mitakatifuⁿ na

33:14 *Au "kwenye korongo." **33:19** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

sanamu za kuchongwa kabla hajajinyenyekeza, mambo hayo yameandikwa katika maandishi ya waonaji wake. **20** Kisha Manase akafa na kuzikwa pamoja na mababu zake nyumbani kwake; na Amoni mwanawe akawa mfalme baada yake.^a

21 Amoni^b alikuwa na umri wa miaka 22 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka miwili huko Yerusalemu.^c **22** Naye aliendelea kute nda maovu machoni pa Yehova, kama alivyofanya Manase baba yake;^d na Amoni akatoa dhahabu kwa sanamu zote za kuchongwa ambazo Manase baba yake alikuwa ametengeza,^e naye akaendelea kuziabudu. **23** Lakini hakujiinyenyekeza mbele za Yehova^f kama Manase baba yake alivyojinyenyekeza;^g badala yake, Amoni alizidisha sana hatia yake. **24** Hatimaye watumishi wake wakapanga njama dhidi yake^h na kumuua ndani ya nyumba yake mwenyewe. **25** Lakini watu wa nchi hiyo wakawaua wale wote waliopanga njama dhidi ya Mfalme Amoni,ⁱ nao wakamweka Yosia mwanawe^j kuwa mfalme baada yake.

34 Yosia^k alikuwa na umri wa miaka minane alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 31 huko Yerusalemu.^l **2** Alitenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova na kutembea katika njia za Daudi babu yake, naye hakugeuka na kwenda kulia au kushoto.

3 Katika mwaka wa 8 wa utawala wake, alipokuwa angali mvulana, alianza kumtafuta Mungu wa Daudi babu

SURA YA 33

a 2Fa 21:18, 19

b Mt 1:10

c 2Fa 21:19-24

d 2Nya 33:1, 2

e 2Fa 21:1, 7

f Yer 8:12

g 2Nya 33:12, 13

h 2Fa 12:20
2Nya 25:27

i 2Nya 25:1, 3

j 2Fa 21:25, 26

SURA YA 34

k 1Fa 13:2

Sef 1:1
Mt 1:10

l 2Fa 22:1, 2

Safu ya 2

a 2Nya 15:2

b 2Fa 23:4, 14

c 2Nya 33:17

d 2Nya 33:21, 22

e 2Fa 23:6

f 1Fa 13:2
2Fa 23:16g 2Fa 23:19
2Nya 30:1

h 2Fa 17:41

i 2Nya 31:1

j 2Fa 22:12

k 2Fa 22:3-6

yake;^a na katika mwaka wa 12, akaanza kusafisha Yuda na Yerusalemu^b kwa kuondoa mahali pa juu^c na miti mitakatifu,^{*} sanamu za kuchongwa,^d na sanamu za chuma.[#] **4** Pia, wali-bomoa madhabahu za Mabaali mbele yake, naye akavikatakata vinara vya uvumba vilivyokuwa juu ya madhabahu hizo. Pia alivunja vipandevipande miti mitakatifu,^{*} sanamu za kuchongwa, na sanamu za chuma,[#] akazipondaponda zikawa ungaunga na kuunyuniyiza juu ya makaburi ya wale waliokuwa wakizitolea dhahabu.^e **5** Akaitekeza mifupa ya makuhani juu ya madhabahu zao.^f Basi akaisafisha nchi ya Yuda na Yerusalemu.

6 Na katika majiji ya Manase, Efraimu,^g Simeoni, na mpaka Naftali, katika magofu yaliyozunguka majiji hayo, **7** alibomoa madhabahu na kupondaponda miti mitakatifu^{*} na sanamu za kuchongwa,^h zikabaki ungaunga; naye akavikatakata vinara vyote vya uvumba katika nchi yote ya Israeli,ⁱ kisha akarudi Yerusalemu.

8 Katika mwaka wa 18 wa utawala wake, alipokuwa ameisafisha nchi na hekalu,^{*} alimtuma Shafaniⁱ mwana wa Azalia, Maaseya mkuu wa jiji, na Yoa mwana wa Yohazi aliyefanya kazi ya kuweka kumbukumbu ili wairekebisha nyumba ya Yehova Mungu wake.^k **9** Walienda kwa kuhani mkuu Hilkia na kumpa pesa zilizokuwa zimeletwa katika nyumba ya Mungu, ambazo Walawi waliokuwa walinzi

34:3, 4, 7 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
34:3, 4 #Au "sanamu za kuyeyushwa."
34:8 *Tnn., "nyumba."

wa malango walikuwa wamekusanya kutoka kwa watu wa kabila la Manase, Efraimu, na Waisraeli wengine wote,^a na pia kutoka kwa watu wa Yuda, Benjamini, na wakaaji wa Yerusalemu. **10** Kisha wakawapa pesa hizo wale waliowekwa kusimamia kazi katika nyumba ya Yehova. Halafu wafanyakazi waliokuwa katika nyumba ya Yehova wakazitumia kuikarabati na kuirekebisha nyumba hiyo. **11** Waliwapa mafundi na wajenzi ili wanunue mawe yaliyochongwa na mbao za kuunganisha na za kutengeneza maboriti wa kujenga nyumba ambazo wafalme wa Yuda waliacha ziharibike.^b

12 Wanaume hao walifanya kazi hiiyo kwa uaminifu.^c Walawi waliowekwa wawasimamie ni Yahathi na Obadia kutoka kwa Wamerari,^d na Zekaria na Meshulamu kutoka kwa Wakohathi,^e ili watumikie wakiwa waangalizi. Na Walawi fulani, ambao wote walikuwa wanamuziki stadi,^f **13** waliwasimamia vibarua* na walikuwa waangalizi wa watu wote waliokuwa wakifanya kazi katika utumishi wa aina mbalimbali; na baadhi ya Walawi walikuwa waandishi, maofisa, na walinzi wa malango.^g

14 Walipokuwa wakitoa pesa zilizokuwa zimeletwa katika nyumba ya Yehova,^h kuhani Hilikia alipata kitabu cha Sheria ya Yehovaⁱ kilichotolewa kupitia* Musa.^j **15** Kwa hiyo Hilikia akamwambia mwandishi Shafani: "Nimepata kitabu cha Sheria katika nyumba ya Yehova." Basi Hilikia akampa Shafani kitabu hicho.

34:13 *Au "waliobeba mizigo." **34:14** *Tnn., "kwa mkono wa."

SURA YA 34

a 2Nya 30:11, 18

b 2Fa 12:11, 12

c 2Fa 12:15

d 1Nya 23:6

e 2Nya 20:19

f 1Nya 25:1

g 2Nya 8:14

h 2Fa 22:4

i Kum 17:18
Kum 31:24-26
Yos 1:8
2Fa 22:8

j Law 26:46

Safu ya 2

a 2Fa 22:8

b Kum 17:18, 19

c 2Fa 22:11-13

d 2Fa 25:22
Yer 40:14e Kum 30:17, 18
Kum 31:16
Kum 31:24-26
Yos 1:8f Kut 15:20
Amu 4:4
Lu 2:36
Mdo 21:8, 9

g 2Fa 22:14-20

16 Kisha Shafani akampelekea mfalme kitabu hicho na kumwambia: "Watumishi wako wanafanya kila jambo ulilowaambia wafanye. **17** Wamekusanya* pesa zilizopatikana katika nyumba ya Yehova, nao wamewapa wanaume waliowekwa kusimamia kazi na wale wanaofanya kazi." **18** Pia, mwandishi Shafani akamwambia mfalme: "Kuna kitabu ambacho kuhani Hilikia amenipa."^a Kisha Shafani akaanza kukisoma mbele ya mfalme.^b

19 Mara tu mfalme aliposikia maneno ya kitabu hicho cha Sheria, akayararua mavazi yake.^c **20** Kisha mfalme akamwagiza hivi Hilikia, Ahikamu^d mwana wa Shafani, Abdoni mwana wa Mika, mwandishi Shafani, na Asaya mtumishi wa mfalme; **21** "Nendeni mkatafute ushauri wa Yehova kwa niaba yangu na kwa niaba ya watu ambao wamebaki Israeli na Yuda kuhusu maneno ya kitabu hiki ambacho kimepatikana; kwa maana ghadhabu ya Yehova itakayomwagwa dhidi yetu ni kali kwa sababu mababu zetu hawakutekeleza neno la Yehova kwa kuyashika mambo yote yaliyoandikwa katika kitabu hiki."^e

22 Basi Hilikia, pamoja na wale waliotumwa na mfalme, wakaenda kwa nabii wa kike aliyetitwa Hulda.^f Alikuwa mke wa Shalumu mwana wa Tikva mwana wa Harhasi, mtunzaji wa chumba cha mavazi, naye alikuwa akiishi katika Wilaya ya Pili ya Yerusalemu; wakazungumza naye huko.^g **23** Akawaambia: "Yehova Mungu wa Israeli anasema

34:17 *Tnn., "Wamemimina."

hivi: ‘Mwambieni hivi mtu aliyewatuma kwangu: **24** “Yehova anasema, ‘Nitaleta msiba mahali hapa na kwa wakaaji wake,^a laana zote zilizozandikwa katika kitabu^b walichosoma mbele ya mfalme wa Yuda. **25** Kwa sababu wameniacha^c na wanafukizia miungu mingine moishi wa dhabihu ili kunikasirisha^d kwa kazi zote za mikono yao, ghadhabu yangu itamwagika mahali hapa nayo haitazimwa.”^e **26** Lakini mwambieni hivi mfalme wa Yuda aliyewatuma kutafuta ushauri wa Yehova: “Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Kuhusu maneno ambayo umezikia,^f **27** kwa sababu moyo wako ulikuwa msikivu,^g nawe ukajinyenyekeza mbele za Mungu uliposikia mambo yake kuhusu mahali hapa na wakaaji wake, ukajinyenyekeza mbele zangu na kuyararua mavazi yako na kulia mbele zangu, mimi pia nimekusikia,^g asema Yehova. **28** Ndiyo sababu nitakuzika pamoja na mababu zako,^h nawe utalazwa kwa amani katika kaburi lako, na macho yako hayataona msiba wote nitakaoleta mahali hapa na kwa wakaaji wake.”^h

Kisha wakampelekea mfalme jibu hilo. **29** Basi mfalme akatuma ujumbe na kuwakusanya wazee wote wa Yuda na Yerusalemu.ⁱ **30** Baada ya hayo mfalme akapanda kwenenda katika nyumba ya Yehova pamoja na wanaume wote wa Yuda, wakaaji wa Yerusalemu, makuhani, Walawi—watu wote, wadogo kwa wakubwa. Akaso-

34:27 *Tnn., “laini.” **34:28** *Tnn., “nitakusanya kwa mababu zako.” Huu ni msemo wa kishairi unaorejelea kifo.

SURA YA 34

a Yer 35:17

b Law 26:16
Kum 28:15
Kum 30:17,18
Da 9:11

c Kum 28:20

d 2Fa 21:1, 3, 6
2Nya 28:1, 3e Kum 29:22, 23
Yer 7:20

f 2Nya 34:19

g 2Nya 32:26
2Nya 33:11, 13h 1Fa 21:29
Isa 39:8

i 2Fa 23:1

Safu ya 2

a 2Fa 23:2
2Nya 17:3, 9
Ne 8:3

b Ezz 10:3

c Kum 6:5

d Kum 31:24-26
2Fa 22:8e 2Nya 30:1, 12
2Nya 33:1, 16

f 2Fa 23:5

SURA YA 35

g Kut 12:3-11
2Fa 23:21

h Kut 12:21

i Law 23:5
Kum 16:1j 2Nya 23:18
2Nya 31:2k Kum 33:10
2Nya 17:8, 9
Ne 8:7, 8l 1Fa 6:38
2Nya 5:7

ma, watu wote wakisikia, maneno yote ya kitabu cha agano kilichokuwa kimepatikana katika nyumba ya Yehova.^a **31** Mfalme akasimama mahali pake na kufanya agano^{*b} mbele za Yehova, kwamba atamfuata Yehova na kushika amri zake, vikumbusho vyake, na masharti yake kwa moyo wake wote na kwa nafsi[#] yake yote^c kwa kutekeleza maneno ya agano hilo yaliyoandikwa katika kitabu hicho.^d **32** Zaidi ya hayo, aliwahimiza watu wote waliokuwa Yerusalemu na Benjamini wakubali agano hilo. Na wakaaji wa Yerusalemu wakatenda kulingana na agano la Mungu, Mungu wa mababu zao.^e **33** Kisha Yosia akaondoa vitu vyote vyenye kuchukiza^{*} katika nchi zote za Waisraeli,^f naye akawafanya watu wote wa Israeli wamtumikie Yehova Mungu wao. Katika maisha yake yote[#] hawakuacha kumfuata Yehova Mungu wa mababu zao.

35 Yosia alifanya sherehe ya Pasaka^g ya Yehova huko Yerusalemu, nao wakamchinja mnyama wa Pasaka^h katika siku ya 14 ya mwezi wa kwanza.ⁱ **2** Aliwaweka makuhani katika zamu zao na kuwatia moyo watekeleze utumishi wao wa nyumba ya Yehova.^j **3** Kisha akawaambia hivi Walawi, walimu wa Waisraeli wote,^k waliokuwa watakatifu kwa Yehova: “Liwekeni Sanduku takatifu ndani ya nyumba ambayo Sulemani mwana wa Daudi mfalme wa Israeli alijenga;^l hampaswi

34:31 *Au “kufanya upya lile agano.”[#] Angalia Kamusi, uku. 2012. **34:33** *Au “akaondoa miungu yote.”[#] Tnn., “Siku zake zote.”

kulibeba tena mabegani mwe-
nu.^a Sasa mtumikieni Yeho-
va Mungu wenu na watu wake
Waisraeli. **4** Na mjitayarisha
kulingana na koo zenu,* kuli-
ngana na vikundi vyenu, mki-
fuata mambo yaliyoandikwa
na Mfalme Daudi^b wa Israe-
li na Sulemani mwanawe.^c
5 Simameni mahali patakati-
fu mkiwa katika vikundi kuli-
ngana na koo* za ndugu zenu,
ambao si Walawi,^d pamoja na
kikundi kinacholingana cha
ukoo* wa Walawi. **6** Mchi-
njeni mnyama wa Pasaka^d na
mjitakase na kufanya mataya-
risho kwa ajili ya ndugu zenu
ili kutekeleza neno la Yehova
kupitia Musa.”

7 Yosia akawachangia watu
wote waliokuwepo makundi
ya kondoo na mbuzi, wana-
kondoo dume na wanambuzi
dume, kwa ajili ya dhabihu za
Pasaka, jumla ya wanakondoo
na wanambuzi 30,000, na pia
ng'ombe 3,000. Wanyama hao
walitolewa katika mali za
mfalme mwenyewe.^e **8** Wa-
kuu wake pia walitoa mcha-
ngo uwe toleo la hiari kwa aji-
li ya watu, makuhani, na Wa-
lawi. Hilikia,^f Zekaria, na Ye-
hieli, viongozi wa nyumba
ya Mungu wa kweli, waliwapa
makuhani wanyama 2,600 wa
dhabihu za Pasaka na ng'o-
mbe 300. **9** Konania na ndu-
gu zake Shemaya na Nethane-
li, pamoja na Hashabia, Yeieli,
na Yozabadi, wakuu wa Wala-
wi, waliwapa Walawi wanya-
ma 5,000 wa dhabihu za Pa-
saka pamoja na ng'ombe 500
kuwa mchango.

10 Matayarisho ya utumishi
huo yakafanywa, na makuha-

35:4, 5, 12 * Yaani, ukoo wa upande wa
baba. 35:5 ^d Tnn., “wana wa watu.”

SURA YA 35

a Hes 4:15
1Nya 23:25, 26

b 1Nya 23:6

c 2Nya 8:14

d Kut 12:21
2Nya 30:1, 15

e 2Nya 30:24

f 2Fa 23:4
2Nya 34:14

Safu ya 2

a 1Nya 23:6

b Kut 12:3, 6

c 2Nya 30:16

d 2Nya 29:34

e Kut 12:8
Kum 16:6, 7

f 1Nya 16:37

g 1Nya 23:5

h 1Nya 25:1, 2

i 1Nya 16:41, 42
1Nya 25:3

j 1Nya 26:12, 13

ni wakasimama mahali pao
na Walawi wakasimama kuli-
ngana na vikundi vyao,^a kama
mfalme alivyokuwa ameamu-
ru. **11** Wakawachinja wanya-
ma wa Pasaka,^b na makuha-
ni wakanyunyiza damu wali-
yopokea kutoka kwao,^c huku
Walawi wakiwachuna ngozi
wanyama hao.^d **12** Kisha wa-
katayarisha dhabihu za kute-
ketezwa ili kuwagawia watu
wasio Walawi, ambao waliku-
wa wamepangwa kulingana na
koo zao,^e ili zitolewe kwa Ye-
hova kama ilivyoandikwa ka-
tika kitabu cha Musa; waka-
fanya vivyo hivyo kwa wale
ng'ombe. **13** Waliipika* dha-
bihi ya Pasaka juu ya moto
kulingana na desturi;^e nao
wakapika matoleo matakatifu
kwenye vyungu, sufuria ku-
bwa, na vikaangio, kisha wa-
kawaletea haraka watu wengi-
ne wote. **14** Kisha wakaita-
yarisha kwa ajili yao wenye-
we na kwa ajili ya makuhani,
kwa sababu makuhani, wazao
wa Haruni, walikuwa wakitoa
dhabihu za kuteketezwa na vi-
pande vyenye mafuta mpaka
giza lilipoingia, kwa hiyo Wa-
lawi wakaitayarisha kwa ajili
yao wenyewe na kwa ajili ya
makuhani, wazao wa Haruni.

15 Na waimbaji, wana wa
Asafu,^f walisimama mahali
pao kama alivyoamuru Da-
udi,^g Asafu,^h Hemani, na
Yeduthuni,ⁱ mwonaji wa mfal-
me; na walinzi wa mala-
ngo walikuwa kwenye mala-
ngo mbalimbali.^j Hawakuhi-
taji kuacha utumishi wao,
kwa sababu ndugu zao Wa-
lawi walikuwa wamewataya-
rishia Pasaka. **16** Kwa hiyo
utumishi wote wa Yehova

35:13 * Au labda, “Walichoma.”

ukatayarishwa siku hiyo ili kuadhimisha Pasaka^a na kutoa dhabihu za kuteketezwa kwenye madhabahu ya Yehova, kulingana na agizo la Mfalme Yosia.^b

17 Waisraeli waliokuwepo waliadhimisha Pasaka wakati huo na pia Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu kwa siku saba.^c **18** Pasaka kama hiyo haikuwa imewahi kuadhimishwa Israeli tangu siku za nabii Samweli; wala wafalme wengine wa Israeli hawakuwa wameadhimisha Pasaka kama hiyo iliyoadhimishwa na Yosia,^d makuhani, Walawi, watu wote wa Yuda na Israeli waliokuwepo, na wakaaji wa Yerusalemu. **19** Pasaka hii ilifanywa katika mwaka wa 18 wa utawala wa Yosia.

20 Baada ya hayo yote, Yosia alipokuwa ametayarisha hekalu,* Mfalme Neko^e wa Misri alipanda kuja kupigana Karkemishi karibu na Mto Efrati. Kisha Yosia akaenda kukabiliana naye.^f **21** Kwa hiyo akamtumia Yosia wajumbe, aki sema: “Vita hivi vinakuhusuje, Ee mfalme wa Yuda? Sijaja kupigana nawe leo, nimekuja kupigana na nyumba nyingine, na Mungu anasema kwamba ninapaswa kufanya haraka. Kwa faida yako mwenyewe, acha kumpinga Mungu, aliye pamoja nami, la sivyo atakuangamiza.” **22** Hata hivyo, Yosia hakugeuka na kumwacha, lakini alibadili sura yake^g ili apigane naye, akakataa kabisa kusikiliza maneno ya Neko, yaliyotoka kinywani mwa Mungu. Basi akaja kupigana naye katika Nchi Tambarare ya Megido.^h

35:20 *Tnn., “nyumba.”

SURA YA 35

a Law 23:5

b 2Fa 23:21

c Kut 12:15
Law 23:6
Kum 16:3
2Nya 30:1, 21

d 2Fa 23:22, 23
2Nya 30:5, 26

e Yer 46:2

f 2Fa 23:29

g 1Fa 22:30

h Amu 1:27
Amu 5:19
Zek 12:11
Ufu 16:16

Safu ya 2

a 2Fa 23:30
2Nya 34:28

b Yer 1:1

c Yer 9:17, 20

d 2Fa 23:28

SURA YA 36

e 1Nya 3:15
Yer 22:11

f 2Fa 23:30, 31

23 Na wapiga mishale wakampiga Mfalme Yosia, akawaambia watumishi wake: “Niondoeni hapa, kwa maana ni-mejeruhiwa vibaya sana.”

24 Kwa hiyo watumishi wake wakamtoa garini, wakamweka kwenye gari lake la pili la vita na kumpeleka Yerusalemu. Kwa hiyo akafa na kuzikwa katika kaburi la mababu zake,^a na watu wote wa Yuda na Yerusalemu wakamwombolezea Yosia. **25** Na Yeremia^b akamwambia Yosia wimbo wa maombolezo, na tangu siku hiyo waimbaji wote wa kiume na wa kike^c wanaendelea kuimba kumhusu Yosia katika nyimbo zao za huzuni,* na uamuzi ukafanywa kwamba nyimbo hizo zinapaswa kumbwa katika nchi ya Israeli, nazo zimeandikwa katika nyimbo za huzuni.

26 Na mambo mengine katika historia ya Yosia na mateendo yake ya upendo mshikamanifu, kulingana na mambo yaliyoandikwa katika Sheria ya Yehova, **27** na mambo aliyofanya, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, yameandikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Israeli na wa Yuda.^d

36 Kisha watu nchini wakamchukua Yehoahazi^e mwana wa Yosia na kumweka kuwa mfalme huko Yerusalemu baada ya baba yake.^f

2 Yehoahazi alikuwa na umri wa miaka 23 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miezi mitatu huko Yerusalemu. **3** Hata hivyo, mfalme wa Misri akamwondoa madakani huko Yerusalemu na kuitoza nchi talanta 100 za fe-

35:25 *Au “maombolezo.”

dha* na talanta moja ya dhababu.^a **4** Zaidi ya hayo, mfalme wa Misri alimweka Eliakimu ndugu ya Yehoahazi kuwa mfalme wa Yuda na Yerusalemu na kubadili jina lake kuwa Yehoyakimu; lakini Neko^b akamchukua Yehoahazi ndugu yake na kumpeleka Misri.^c

5 Yehoyakimu^d alikuwa na umri wa miaka 25 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 11 huko Yerusalemu. Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova Mungu wake.^e **6** Mfalme Nebukadneza^f wa Babiloni alipanda kuja kumshambulia, akamfunga kwa pingu mbili za shaba na kumpeleka Babiloni.^g **7** Pia Nebukadneza alichukua baadhi ya vyombo vya nyumba ya Yehova, akavipeleka Babiloni na kuviweka katika jumba lake la kifalme huko Babiloni.^h **8** Na mambo mengine katika historia ya Yehoyakimu, mambo yenye kuchukiza aliyotenda na mambo yasiyofaa yaliyopatikana dhidi yake, yameandikwa katika Kitabu cha Wafalme wa Israeli na wa Yuda; na Yehoyakini mwanawe akawa mfalme baada yake.ⁱ

9 Yehoyakini^j alikuwa na umri wa miaka 18 alipoanza kutawala, alitawala kwa miezi mitatu na siku kumi huko Yerusalemu; naye aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova.^k **10** Mwanzoni mwa mwaka,^l Mfalme Nebukadneza aliagiza aletwe Babiloni,^m pamoja na vyombo vyenye

36:3 *Talanta moja ilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B4.
36:10 *Labda, majira ya kuchipua.

thamani vya nyumba ya Yehova.^a Akamweka Sedekia ndugu ya baba yake kuwa mfalme wa Yuda na Yerusalemu.^b

11 Sedekia^c alikuwa na umri wa miaka 21 alipoanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 11 huko Yerusalemu.^d

12 Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova Mungu wake. Hakujiinyenyekeza mbele ya nabii Yermia,^e aliyesema mambo aliyogizwa na Yehova. **13** Pia alimwasi Mfalme Nebukadneza,^f aliyekuwa amemwapisha kwa jina la Mungu, akaendelea kuwa mkaidi* na mwenye moyo mgumu na kukataa kumgeukia Yehova Mungu wa Israeli. **14** Wakuu wote wa makuhani na pia watu walikosa uaminifu kupita kiasi, wakitenda mambo yote yenye kuchukiza ya mataifa, nao wakaichafua nyumba ya Yehova^g aliyokuwa ameitakasa Yerusalemu.

15 Yehova Mungu wa mababu zao aliendelea kuwaonya kupitia wajumbe wake, aliwaoonya tena na tena, kwa sababu aliwahirumia watu wake na makao yake. **16** Lakini walielekea kuwadhihaki wajumbe wa Mungu wa kweli,^h wakadharau maneno yakeⁱ na kuwajekeli manabii wake,^j mpaka ghadhabu ya Yehova ilipokuja dhidi ya watu wake,^k hivi kwamba hawangeweza kuponywa.

17 Kwa hiyo akamleta mfalme wa Wakaldayo awashambulie,^l ambaye aliwaua wanaume wao vijana kwa upanga^m katika nyumba ya mahali pao patakatifu;ⁿ hakumhurumia kijana wa kiume wala

36:13 *Tnn., "akafanya shingo yake iwe ngumu."

SURA YA 36

a 2Fa 18:14

2Fa 23:33

b 2Fa 23:29

Yer 46:2

c 2Fa 23:34

Yer 22:11, 12

d Yer 26:20, 21

Yer 36:32

e 2Fa 23:36, 37

f 2Fa 24:1

2Fa 25:1

Yer 25:1

g 2Fa 24:16

Da 1:1

h Ezz 1:7

Yer 27:16

Da 1:2

Da 5:2

i 2Fa 24:5, 6

j Yer 22:24

Mt 1:12

k 2Fa 24:8, 9

l 2Fa 24:10

Yer 29:1, 2

Eze 1:2

Safu ya 2

a 2Fa 24:13

Yer 27:17, 18

b 2Fa 24:17

c Yer 37:1

d 2Fa 24:18-20

Yer 52:1-3

e Yer 21:1, 2

Yer 34:2

Yer 38:14, 24

f 2Fa 24:20

Eze 17:12-15

g 2Fa 16:11

Eze 8:10, 11

h 2Nya 30:1, 10

i Yer 5:12

j Yer 20:7

k Zb 74:1

l 2Fa 24:2

m Law 26:31

Kum 28:25

Zb 79:2

n Eze 9:7

bikira, mzee wala aliye dhai-fu.^a Mungu alitia kila kitu mikononi mwake.^b **18** Alipeleka kila kitu Babiloni, vyombo vyote vya nyumba ya Mungu wa kweli, vikubwa na vido-go, na pia hazina za nyumba ya Yehova na hazina za mfalme na wakuu wake.^c **19** Alii-teketeza kabisa nyumba ya Mungu wa kweli,^d akaubomoa ukuta wa Yerusalemu,^e akateketeza kwa moto minara yake yote yenye ngome, na kuha-ribu kila kitu chenye thamani.^f **20** Aliwachukua mateka na kuwapeleka Babiloni wale ambao hawakuuawa kwa upa-nga,^g nao wakawa watumishi wake^h na wa wanawe mpaka ufalme wa Uajemi ulipoa-nza kutawala,ⁱ **21** ili kutimi-za neno la Yehova lililosemwa

SURA YA 36

- a Omb 2:21
 b Kum 28:49-51
 c 2Fa 20:16, 17
 Isa 39:6
 Yer 27:19-22
 Yer 52:17
 d Zb 74:4-7
 e Yer 52:14
 f 1Fa 9:7
 2Fa 25:9, 10
 Zb 79:1
 g 2Fa 25:21
 Zb 137:1
 h Yer 27:6, 7
 i Ezr 1:1-3

Safu ya 2

- a Yer 25:9
 b Law 26:34
 c Yer 25:12
 Zek 1:12
 d Isa 44:28
 Isa 45:1
 e Yer 29:14
 Yer 32:42
 Yer 33:10, 11
 f Ezr 1:1-4
 g Da 5:18
 h Isa 44:28
 i Ezr 7:12, 13

na Yereimia,^a mpaka nchi ilipo-lipa sabato zake.^b Sikuzote ili-pokuwa ukiwa ilishika sabato, ili kutimiza miaka 70.^c

22 Katika mwaka wa kwa-nza wa utawala wa Mfalme Koreshi^d wa Uajemi, ili neno la Yehova lililosemwa na Ye-remia^e litimie, Yehova aliicho-chea roho ya Mfalme Ko-reshi wa Uajemi atoe tanga-zo katika ufalme wake wote, ambalo pia aliliandika,^f akise-ma: **23** “Mfalme Koreshi wa Uajemi anasema hivi: ‘Yeho-va Mungu wa mbinguni ame-nipa falme zote za dunia,^g naye ameniagiza nimjengee nyumba Yerusalemu, nchini Yuda.^h Yeyote miongoni mwe-nu, ninyi watu wake wote, Ye-hova Mungu wake na awe pa-moja naye, na apande kwenda huko.’”ⁱ

EZRA

YALIYOMO

- | | |
|---|--|
| <p>1 Agizo la Mfalme Koreshi la kujenga upya hekalu (1-4)
Watu walio uhamishoni wajitayarisha kurudi Babiloni (5-11)</p> <p>2 Orodha ya watu waliorudi kutoka uhamishoni (1-67)
Watumishi wa hekaluni (43-54)
Wana wa watumishi wa Sulemani (55-57)
Matoleo ya hiari kwa ajili ya hekalu (68-70)</p> <p>3 Madhabahu yajengwa upya na dhabihu zatolewa (1-6)
Kazi ya kujenga upya hekalu yaanza (7-9)
Msingi wa hekalu wawekwa (10-13)</p> <p>4 Kazi ya kujenga upya hekalu yapingwa (1-6)</p> | <p>Maadui watuma malalamishi kwa Mfalme Artashasta (7-16)
Artashasta ajibu (17-22)
Ujenzi wa hekalu wasimamishwa (23, 24)</p> <p>5 Wayahudi waanza tena kujenga hekalu (1-5)
Barua ambayo Tatenai alimtumia Mfalme Dario (6-17)</p> <p>6 Uchunguzi na agizo la Dario (1-12)
Ujenzi wakamilika na hekalu lazinduliwa (13-18)
Pasaka yaadhimishwa (19-22)</p> <p>7 Ezra aja Yerusalemu (1-10)
Barua ya Artashasta kwa Ezra (11-26)
Ezra amsifu Yehova (27, 28)</p> <p>8 Orodha ya wale waliorudi pamoja na Ezra (1-14)</p> |
|---|--|

Maandalizi ya safari (15-30)
Kuondoka Babiloni na kufika
Yerusalemu (31-36)

- 9 Waisraeli waoa wanawake wa
kigeni (1-4)
Sala ya Ezra za kuungama (5-15)

- 10 Agano la kuwafukuza
wanawake wa kigeni (1-14)
Wanawake wa kigeni
wafukuzwa (15-44)

1 Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Mfalme Koreshi^a wa Uajemi, ili neno la Yehova lililosemwa na Yermia^b litimie, Yehova aliichochea roho ya Mfalme Koreshi wa Uajemi atoe tangazo katika ufalme wake wote, ambalo pia aliliandika,^c akisema:

2 “Mfalme Koreshi wa Uajemi anasema hivi: ‘Yehova Mungu wa mbinguni amenipa falme zote za dunia,^d naye ameniagiza nimjengee nyumba Yerusalemu, nchini Yuda.’^e

3 Yeyote miongoni mwenu, ninyi watu wake wote, Mungu wake na awe pamoja naye, na apande kwenda Yerusalemu, kule Yuda, na kuijenga upya nyumba ya Yehova Mungu wa Israeli—yeye ndiye Mungu wa kweli—ambaye nyumba yake ilikuwa Yerusalemu.* **4** Na mkaaji mgeni yeyote,^f popote alipo, majirani zake* wamsaidie kwa kumpa fedha na dhahabu, mali na wanyama wa kufugwa, pamoja na toleo la hiari kwa ajili ya nyumba ya Mungu wa kweli,^g iliyokuwa Yerusalemu.”

5 Ndipo viongozi wa ukoo* wa Yuda na Benjamini na makuhani na Walawi—kila mmoja

1:3 *Au labda, “aliye Yerusalemu.” 1:4 *Tnn., “watu wa mahali pake.” 1:5 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 1

a Isa 45:1
Da 10:1

b Yer 25:12
Yer 29:14
Yer 33:10, 11

c 2Nya 36:22, 23

d Da 4:34, 35

e Isa 44:28

f 2Fa 17:6
Yer 9:16

g Kut 35:21
1Nya 29:9
Ezr 7:14-16

Safu ya 2

a 2Fa 24:11, 13
2Nya 36:7, 18
Ezr 6:5
Da 1:1, 2
Da 5:2

b Ezr 5:14, 16
Hag 1:1, 14
Hag 2:23

ambaye roho yake ili chochea na Mungu wa kweli—waka-jitayarisha kupanda kwenda kujenga upya nyumba ya Yehova, iliyokuwa Yerusalemu. **6** Wale wote waliowazunguka wakawasaidia kwa kuwapa* vyombo vya fedha na dhahabu, mali, wanyama wa kufugwa, na vitu vyenye thamani, mbali na matoleo yote ya hiari.

7 Pia, Mfalme Koreshi akaleta vyombo vya nyumba ya Yehova ambavyo Nebukadneza alikuwa amechukua huko Yerusalemu na kuviweka katika nyumba ya mungu wake.^a

8 Mfalme Koreshi wa Uajemi akavikabidhi kwa Mithredathi mweka-hazina ambaye alivihesabu na kumpa Sheshbazarⁱ*^b mkuu wa Yuda.

9 Hii ndiyo idadi yake: vyombo 30 vya dhahabu vyenye umbo la kikapu, vyombo 1,000 vya fedha vyenye umbo la kikapu, vyombo 29 vya akiba, **10** mabakuli madogo 30 ya dhahabu, mabakuli madogo 410 ya fedha, vyombo vingine 1,000. **11** Vyombo vyote vya dhahabu na vya fedha vilikuwa 5,400. Sheshbazarⁱ alivibeba vyote wakati yeye

1:6 *Tnn., “wakaitia nguvu mikono yao kwa.” 1:8 *Labda ni Zerubabeli anayetajwa kwenye Ezr 2:2; 3:8.

na watu waliohamishwa^a walipoondoka Babiloni kwenda Yerusalemu.

2 Hawa ndio watu wa mkoa,* baadhi ya mateka waliopanda kutoka uhamishoni,^b ambao Mfalme Nebukadneza wa Babiloni alikuwa amewapeleka uhamishoni Babiloni^c na ambao baadaye walirudi Yerusalemu na Yuda, kila mmoja kwenye jiji lake,^d **2** wale waliokuja na Zerubabeli,^e Yeshua,^f Nehemia, Sera-ya, Reelaya, Mordekai, Bilshani, Mispari, Bigvai, Rehumu, na Baana.

Idadi ya wanaume Waisraeli ilitia ndani:^g **3** wana wa Paroshi, 2,172; **4** wana wa Shefatia, 372; **5** wana wa Ara,^h 775; **6** wana wa Pahathmoabu,ⁱ wa wana wa Yeshua na Yoabu, 2,812; **7** wana wa Elamu,^j 1,254; **8** wana wa Zatu,^k 945; **9** wana wa Zakai, 760; **10** wana wa Bani, 642; **11** wana wa Bebai, 623; **12** wana wa Azgadi, 1,222; **13** wana wa Adonikamu, 666; **14** wana wa Bigvai, 2,056; **15** wana wa Adini, 454; **16** wana wa Ateri, wa Hezekia, 98; **17** wana wa Besai, 323; **18** wana wa Yora, 112; **19** wana wa Hashumu,^l 223; **20** wana wa Gibari, 95; **21** wana wa Bethlehemu, 123; **22** wanaume wa Netofa, 56; **23** wanaume wa Anathothi,^m 128; **24** wana wa Azmavethi, 42; **25** wana wa Kiriath-yearimu, Kefira na Beerothi, 743; **26** wana wa Ramaⁿ na Geba,^o 621; **27** wanaume wa Mikmasi, 122; **28** wa-

2:1 * Au "wilaya ya utawala."

SURA YA 1

a 2Fa 24:14, 15
2Nya 36:20

SURA YA 2

b Ezr 8:1

c 2Fa 24:15, 16
2Fa 25:11
2Nya 36:20

d Ne 7:6, 7

e Ezr 1:8, 11
Hag 1:14
Mt 1:12

f Ezr 3:8
Ezr 5:2
Zek 3:1

g Ne 7:8-38

h Ne 6:17, 18

i Ezr 10:30, 44
Ne 3:11

j Ezr 10:26, 44

k Ezr 10:27, 44

l Ezr 10:33, 44

m Yos 21:8, 18
Yer 1:1

n Yos 18:21, 25

o Yos 18:21, 24

Safu ya 2

a Yos 7:2

b Ezr 10:43, 44

c Ne 7:39-42

d 1Nya 9:2, 10
Ne 11:3, 10

e 1Nya 24:3, 11

f 1Nya 24:3, 14
Ezr 10:20, 44

g Ezr 10:22, 44

h 1Nya 24:3, 8
Ezr 10:21, 44

i Ne 7:43

j Ezr 3:9
Ne 12:8, 24

k Ne 7:44

l 1Nya 15:16, 17
Ne 11:3, 17

m Ne 7:45

n 1Nya 9:2, 17
Ne 11:3, 19

o Ne 12:25, 26

p Yos 9:3, 27
1Nya 9:2
Ne 3:26
Ne 7:46-56

naume wa Betheli na Ai,^a 223; **29** wana wa Nebo,^b 52; **30** wana wa Magbishi, 156; **31** wana wa Elamu mwingine, 1,254; **32** wana wa Harimu, 320; **33** wana wa Lodi, Hadi-di na Ono, 725; **34** wana wa Yeriko, 345; **35** wana wa Senaa, 3,630.

36 Makuhani:^c wana wa Yedayu^d wa nyumba ya Yeshua,^e 973; **37** wana wa Imeri,^f 1,052; **38** wana wa Pashuri,^g 1,247; **39** wana wa Harimu,^h 1,017.

40 Walawi:ⁱ wana wa Yeshua na Kadmieli,^j wa wana wa Hodavia, 74. **41** Waimbajji:^k wana wa Asafu,^l 128. **42** Wana wa walinzi wa malango:^m wana wa Shalumu, wana wa Ateri, wana wa Talmoni,ⁿ wana wa Akubu,^o wana wa Hatita, wana wa Shobai, wote pamoja walikuwa 139.

43 Watumishi wa hekaluni:^{*p} wana wa Siha, wana wa Hasufa, wana wa Tabaothi, **44** wana wa Kerosi, wana wa Siaha, wana wa Padoni, **45** wana wa Lebana, wana wa Hagaba, wana wa Akubu, **46** wana wa Hagabu, wana wa Salmi, wana wa Hanani, **47** wana wa Gideli, wana wa Gahari, wana wa Reaya, **48** wana wa Resini, wana wa Nekoda, wana wa Gazamu, **49** wana wa Uza, wana wa Pasea, wana wa Besai, **50** wana wa Asna, wana wa Meunimu, wana wa Nefusimu, **51** wana wa Bakbuki, wana wa Hakufa, wana wa Harhuri, **52** wana wa Basluthi, wana wa Mehida, wana

2:43 * Au "Wanethini." Tnn., "Waliotolewa."

wa Harsha, **53** wana wa Bar-kosi, wana wa Sisera, wana wa Tema, **54** wana wa Nezia, wana wa Hatifa.

55 Wana wa watumishi wa Sulemani: wana wa Sotai, wana wa Soferethi, wana wa Peruda,^a **56** wana wa Yaala, wana wa Darkoni, wana wa Gideli, **57** wana wa She-fatia, wana wa Hatili, wana wa Pokereth-hazebaimu, wana wa Ami.

58 Watumishi wote wa hekaluni* na wana wa watumishi wa Sulemani walikuwa 392.

59 Na hawa ndio waliopanda kutoka Tel-mela, Tel-harsha, Kerubi, Adoni, na Imeri, lakini hawakuweza kuthibitisha kama ukoo wao* na asili yao ilikuwa ya Waisraeli:^b **60** wana wa Delaya, wana wa Tobia, wana wa Nekoda, **652**. **61** Na kutoka kwa wana wa makuhani: wana wa Habaya, wana wa Hakozi,^c wana wa Barzilai, aliyemwoa mmoja kati ya mabinti wa Barzilai^d Mgileadi na kuitwa kwa jina lao. **62** Hao walichunguza kumbukumbu zao ili wathibitisha ukoo wao, lakini hawakupata majina ya koo zao, kwa hiyo hawakustahili kuwa makuhani.*^e **63** Gavana* akawaambia kwamba hawangeweza kula vitu vitakatifu kabisa^f mpaka apatikane kuhani ambaye angechunguza Urimu na Thumimu.^g

64 Kutaniko lote lilikuwa na jumla ya watu 42,360,^h

2:58 *Au "Wanethini." Tnn., "Waliotolewa." 2:59, 68 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 2:62 *Au "hawakustahili utumishi wa kikuhani kwa sababu hawakuwa safi." 2:63 *Au "Tirshatha," cheo cha Kijemi cha gavana wa mkoa.

SURA YA 2

a Ne 7:57-60

b Ne 7:61-65

c 1Nya 24:3, 10
Ne 3:21d 2Sa 17:27-29
1Fa 2:7

e Hes 3:10

f Law 2:3
Law 6:26
Hes 18:11g Kut 28:30
Hes 27:21
1Sa 28:6h Ne 7:66-69
Isa 10:21
Yer 23:3

Safu ya 2

a Kut 35:5
1Nya 29:5
Ne 7:70-72

b 2Nya 3:1

c Ezr 8:25

d Ne 7:73

SURA YA 3

e 1Fa 8:2

f Hag 1:1

g Ezr 1:7, 8
Lu 3:23, 27h 1Nya 3:17
Mt 1:12

65 mbali na watumwa wao wa kiume na wa kike, ambao walikuwa 7,337; walikuwa pia na waimbaji 200 wa kiume na wa kike. **66** Walikuwa na farasi 736, nyumbu 245, **67** ngamia 435, na punda 6,720.

68 Walipofika kwenye nyumba ya Yehova kule Yerusalemu, baadhi ya viongozi wa koo* wakatoa matoleo ya hiari^a kwa ajili ya nyumba ya Mungu wa kweli, ili kujenga upya[#] mahali ilipokuwa.^b **69** Kulingana na uwezo wao walitoa mchango kwa ajili ya hazina ya kazi, drakma 61,000 za dhahabu,* na mina 5,000 za fedha,^{#c} na kanzu 100 za makuhani. **70** Na makuhani, Walawi, baadhi ya watu, waimbaji, walinzi wa malango, na watumishi wa hekaluni,* wakaanza kuishi katika majiji yao. Na Waisraeli wengine wote[#] wakaanza kuishi katika majiji yao.^d

3 Mwezi wa saba^e ulipofika Waisraeli* walikuwa katika majiji yao; wakakusanyika Yerusalemu wakiwa na kusudi moja. **2** Yeshua^f mwana wa Yehosadaki na makuhani wenzake na Zerubabeli^g mwana wa Shealtieli^h na ndugu zake wakasimama na kujenga madhabahu ya Mungu wa

2:68 #Au "kuisimamisha." 2:69 *Kwa kawaida drakma ilikuwa sawa na dariki ya dhahabu wa Uajemi yenye uzito wa gramu 8.4. Si drakma ya Maandiko ya Kigiriki. Angalia Nyongeza B14. #Mina inayotajwa katika Maandiko ya Kiebrania ilikuwa na uzito wa gramu 570. Angalia Nyongeza B14. 2:70 *Au "Wanethini." Tnn., "waliotolewa." #Tnn., "Waisraeli wote." 3:1 *Tnn., "wana wa Israeli."

Israeli, ili kutoa dhabihu za kuteketezwa juu yake, kama ilivyoandikwa katika Sheria ya Musa,^a mtu wa Mungu wa kweli.

3 Basi wakajenga madhabahu mahali ilipokuwa zamani, ingawa waliwaogopa watu wa nchi jirani,^b nao wakaanza kumtolea Yehova dhabihu za kuteketezwa juu yake, asubuhi na jioni.^c **4** Kisha wakafanya Sherehe ya Vibanda* kulingana na ilivyoandikwa,^d na siku baada ya siku walitoa idadi iliyohitajika ya dhabihu za kuteketezwa.^e **5** Baadaye walitoa dhabihu za kuteketezwa zilizotolewa kwa ukawaida^f na matoleo kwa ajili ya miezi mipya^g na majira yote yaliyotakaswa^h ya sherehe za Yehova, na pia toleo la hiari la kila mtu aliyemtolea Yehova kwa kupeenda.ⁱ **6** Tangu siku ya kwanza ya mwezi wa saba,^j walianza kumtolea Yehova dhabihu za kuteketezwa, ingawa bado msingi wa hekalu la Yehova haukuwa umewekwa.

7 Wakawapa pesa wakataji wa mawe^k na mafundi,^l na kuwapa Wasidoni na Watiro vyakula na vinywaji na mafuta ili walete mbao za mieriye kupitia bahari kutoka Lebanoni mpaka Yopa,^m kwa ruhusa ya Mfalme Koreshi wa Uajemi.ⁿ

8 Katika mwaka wa pili tangu walipofika kwenye nyumba ya Mungu wa kweli huko Yerusalemu, katika mwezi wa pili, Zerubabeli mwana wa Shealtieli, Yeshua mwana wa Yehosadaki na ndugu zao wote, makuhani na Walawi, na wale wote waliorudi

SURA YA 3

a Kut 20:24
Kut 40:29

b Ezz 4:4

c Hes 28:3, 4

d Kut 23:16
Law 23:34

e Kut 29:38
Hes 29:12, 13

f Kut 29:39, 42

g Hes 10:10
Zb 81:3

h Kum 16:16

i Kum 12:5, 6

j Hes 29:1

k 1Fa 5:17

l Ezz 5:8

m Yos 19:46, 48
1Nya 22:3, 4
2Nya 2:10, 16

n Ezz 1:2, 3
Ezz 6:3, 4

Safu ya 2

a Ne 7:6, 7

b Ne 3:18

c Zek 4:9

d Hes 10:8

e 1Nya 6:31, 32
1Nya 23:5
1Nya 25:1

f Kut 15:21
Ne 12:24

g 1Nya 16:34
2Nya 7:3

h 1Fa 6:22
Hag 2:3

i Zb 126:1, 6
Isa 35:10
Zek 4:9

Yerusalemu kutoka utekwani^a wakaanza kazi; wakawaweka rasmi Walawi kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi wawe wasimamizi wa kazi ya nyumba ya Yehova. **9** Basi Yeshua, wanawe na ndugu zake, na Kadmieli na wanawe, wana wa Yuda, wakaungana ili kuwasimamia wale waliokuwa wakifanya kazi katika nyumba ya Mungu wa kweli, pamoja na wana wa Henadi,^b wana wao na ndugu zao Walawi.

10 Wajenzi walipoweka msingi wa hekalu la Yehova,^c makuhani waliovaa mavazi rasmi, wakiwa na tarumbeta,^d na Walawi, wana wa Asafu, wakiwa na matoazi, wakasi-mama ili kumsifu Yehova kulingana na maagizo ya Mfalme Daudi wa Israeli.^e **11** Nao wakaanza kuimba kwa kuitikia^f wakimsifu na kumshukuru Yehova "kwa maana yeye ni mwema; upendo wake mshikamanifu kwa Israeli unadumu milele."^g Kisha watu wote wakapaza sauti wakimsifu Yehova kwa sababu msingi wa nyumba ya Yehova ulikuwa umewekwa. **12** Makuhani wengi, Walawi, na viongozi wa koo*—wazee ambao walikuwa wameona ile nyumba ya kwanza^h—wakalia kwa sauti kubwa walipoona msingi wa nyumba hii ukiwekwa, na wengine wengi wakapaza sauti yao yote kwa shangwe.ⁱ **13** Hivyo watu hawakuweza kutofautisha kati ya sauti ya kushangilia na ya kulia, kwa maana watu walikuwa wakipaza sauti kubwa hivi kwa-

3:4 *Au "Vibanda vya Muda."

3:12 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

mba sauti hiyo ikasikika mbali sana.

4 Maadui wa Yuda na Benjamini^a waliposikia kwamba watu waliorudi kutoka uhamishoni^b walikuwa wakimjengea hekalu Yehova Mungu wa Israeli, **2** mara moja wakamfikia Zerubabeli na viongozi wa koo* na kuwaambia: "Acheni tujenge pamoja nanyi; kwa maana, sisi pia tunamwabudu^c Mungu wenu^c na tumekuwa tukimtolea dhambi hangu siku za Mfalme Esarhadoni^d wa Ashuru, aliyetuleta hapa."^e **3** Hata hivyo, Zerubabeli na Yeshua na viongozi wa koo* za Israeli wakawaambia: "Hamna haki ya kujenga pamoja nasi nyumba ya Mungu wetu,^f kwa maana sisi wenyewe tutamjengea Yehova Mungu wa Israeli, kama alivyotumuru Mfalme Koreshi, mfalme wa Uajemi."^g

4 Ndipo watu wa mataifa jirani wakazidi kuwavunja moyo* watu wa Yuda na kuwakatisha tamaa ili wasijenge.^h **5** Waliwakodi washauri ili kuvuruga mipango yao ya kujenga,ⁱ siku zote za Mfalme Koreshi wa Uajemi mpaka wakati wa utawala wa Mfalme Darío^j wa Uajemi. **6** Mwanzoni mwa utawala wa Ahasuero, waliandika mashtaka dhidi ya wakaaji wa Yuda na Yerusalemu. **7** Na katika siku za utawala wa Mfalme Artashasta wa Uajemi, Bishlamu, Mithredathi, Tabeeli, na wenzake walimwandikia Mfalme Artashasta; wakaitafsiri barua hiyo

4:2, 3 * Yaani, ukoo wa upande wa baba. 4:2 * Tnn., "tunamtafuta." 4:4 * Tnn., "kuilegeza mikono ya."

SURA YA 4

a Ezr 4:6-8
Ne 4:7, 8

b Ezr 2:1, 64

c 2Fa 17:33, 34

d 2Fa 19:36, 37

e 2Fa 17:24

f Ne 2:19, 20
Yoh 4:9, 22

g 2Nya 36:23
Ezr 1:1-3
Ezr 6:3, 4

h Ne 6:9

i Ne 6:10-12

j Ezr 4:24
Ezr 5:5
Ezr 6:1

Safu ya 2

a 2Fa 18:26

b Mwa 10:9, 10

c Ne 1:1
Est 1:2
Da 8:2

d Mwa 10:22
Isa 11:11
Yer 49:35, 36

e 2Fa 17:24

f Ne 1:3

g 2Fa 23:35
Ne 5:4

katika Kiaramu,^a na kuiandika kwa herufi za Kiaramu.*

8 * Rehumu ofisa mkuu wa serikali na mwandishi Shimshai, walimwandikia Mfalme Artashasta barua ifuatayo dhidi ya Yerusalemu: **9** (Ilitoka kwa Rehumu ofisa mkuu wa serikali na mwandishi Shimshai na wenzao, yaani, waamuzi na magavana wadogo, waandishi, watu wa Ereki,^b Wababiloni, wakaaji wa Susa,^c yaani, Waelamu,^d **10** na mataifa mengine yote ambayo Asenapari mkuu na mheshimiwa aliwahamisha na kuwapeleka katika majiji ya Samaria,^e na wengine walio Ng'ambo ya Mto,* basi sasa **11** hii ndiyo nakala ya barua waliyomtumia.)

"Kwa Mfalme Artashasta kutoka kwa watumishi wako, watu walio Ng'ambo ya Mto: Sasa **12** tungependa kumjulisha mfalme kwamba Wayahudi waliokuja huku kutoka kwako wamefika Yerusalemu. Wanajenga upya lile jiji lenye uasi na uovu, nao wanamaliza kujenga kuta^f na kurekebisha misingi yake. **13** Sasa tungependa mfalme ajue kwamba ikiwa jiji hili litajengwa upya na kuta zake kukamilishwa, hawatalipa kodi, ushuru,^g wala ada, na jambo hilo litasababisha hasara kwa hazina za wafalme. **14** Na kwa kuwa sisi hula chumvi ya jumba la mfalme* na

4:7 * Au labda, "iliandikwa katika Kiaramu kisha ikatafsiriwa." 4:8 * Mwanzoni, maandishi ya Ezr 4:8 hadi 6:18 yaliandikwa katika Kiaramu. 4:10 * Au "maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati." 4:14 * Au "tunapokea mshahara wetu kutoka kwenye makao ya mfalme."

si vema kwetu kuona masilahi ya mfalme yakiathiriwa, ndiyo sababu tumetuma barua ili kumjulisha mfalme jambo hilo, **15** ili uchunguzi ufanywe katika kitabu cha kumbukumbu za mababu zako.^a Ndipo utakapona katika kitabu hicho cha kumbukumbu kwamba hili ni jiji lenye uasi, linalowaletea hasara wafalme na mikoa,* na tangu zamani lilikuwa na wachochezi wa uasi. Ndiyo sababu jiji hili liliangamizwa.^b **16** Tunakujulisha mfalme kwamba jiji hili likijengwa upya na kuta zake kukamilishwa, hutaweza kutawala tena* eneo lililo Ng'ambo ya Mto."^c

17 Mfalme akatuma ujumbe ufuatao kwa Rehumu ofisa mkuu wa serikali na mwandishi Shimshai na wenzao waliishi Samaria na katika eneo lote lililo Ng'ambo ya Mto:

"Salamu! Na sasa **18** barua rasmi mliyotutumia imesomwa waziwazi* mbele yangu. **19** Niliagiza uchunguzi ufanywe na ikajulikana kwamba tangu zamani jiji hilo limekuwa na uchochezi na uasi.^d **20** Kulikuwa na wafalme wenyewe nguvu juu ya Yerusalemu waliotawala eneo lote la Ng'ambo ya Mto, nao walikuwa wakilipwa kodi, ushuru, na ada. **21** Sasa toeni amri ili kusimamisha kazi ya wanau-me hao, ili jiji hilo lisijengwe upya mpaka nitakapotoa agizo. **22** Hakikisheni amri hii

4:15 *Au "wilaya za utawala." 4:16 *Tnn., "hutakuwa na fungu katika." 4:18 *Au labda, "imetafsiriwa na kusomwa."

SURA YA 4

a Est 2:23
Est 6:1

b Yer 52:3

c Kum 11:24

d 2Fa 18:1, 7
2Fa 24:20
Ezr 4:15

Safu ya 2

a Ezr 4:13

b Ezr 5:5
Ezr 6:1
Hag 1:14, 15

SURA YA 5

c Hag 1:1

d Zek 1:1

e Ne 12:1, 4

f Mt 1:12

g Zek 6:11

h Ezr 3:2, 8

i Ezr 6:14
Hag 2:4, 21
Zek 4:7

j Ezr 7:6, 28
Ezr 8:22

inatekelezwa bila uzembe, ili masilahi ya mfalme yasiendelee kuathiriwa."^a

23 Sasa baada ya nakala ya barua rasmi ya Mfalme Artashasta kusomwa mbele ya Rehumu na mwandishi Shimshai na wenzao, mara moja wakazinda Yerusalemu na kuwalazimisha Wayahudi waache kujenga. **24** Ndipo kazi ya kujenga nyumba ya Mungu, iliyokuwa Yerusalemu, iliposimamishwa; na haikuendelea mpaka mwaka wa pili wa utawala wa Mfalme Dario wa Uajemi.^b

5 Ndipo nabii Hagai^c na nabii Zekaria,^d mjukuu wa Ido^e wakawatabiria Wayahudi waliokuwa Yuda na Yerusalemu, katika jina la Mungu wa Israeli aliyekuwa akiwaongoza. **2** Kisha Zerubabeli^f mwana wa Shealtieli na Yeshua^g mwana wa Yehosadaki wakaanza kujenga upya nyumba ya Mungu,^h iliyokuwa Yerusalemu; na manabii wa Mungu walikuwa pamoja nao na waliwatia moyo.ⁱ

3 Wakati huo Tatenai gavana wa eneo lililo Ng'ambo ya Mto* na Shethar-bozenai na wenzao wakaja na kuwauliza: "Ni nani aliyewaagiza mjenge nyumba hii na kukamilisha nguzo hizi?"[#] **4** Pia, wakaauliza: "Wanaume wanaojenga jengo hili ni akina nani?" **5** Lakini Mungu alikuwa pamoja na* wazee wa Wayahudi,^j nao hawangeweza kuwazuia kabla ya kumwandikia Dario

5:3 *Au "maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati." #Au "mihimili hii." 5:5 *Tnn., "macho ya Mungu wao yalikuwa juu ya."

na kupata barua rasmi kuhusu jambo hilo kutoka kwake.

6 Hii ndiyo nakala ya barua ambayo Tatenai gavana wa eneo lililo Ng'ambo ya Mto na Shethar-bozenai na wenzake, magavana wadogo wa eneo lililo Ng'ambo ya Mto, walimtumia Mfalme Dario; **7** walimtumia habari hiyo, na hivi ndivyo walivyoandika:

“Kwa Mfalme Dario:

“Na uwe na amani nyingi! **8** Tungependa kumjulisha mfalme kwamba tulienda katika mkoa* wa Yuda kwenye nyumba ya yule Mungu mkuu, nayo inajengwa kwa mawe makubwa yaliyobingirishwa na kuwewa mahali pake, na mbao zinawekwa katika kuta. Watu hao wanafanya kazi hiyo kwa bidii na inasonga mbele kwa jitihada zao. **9** Ndipo tukawauliza wazee wao: ‘Ni nani aliyewaagiza mjenje nyumba hii na kukamilisha nguzo hizi?’*^a **10** Pia, tuliwauliza majina yao ili tuandike majina ya viongozi wao na kukujulisha.

11 “Walitujibu hivi: ‘Sisi ni watumishi wa Mungu wa mbingu na dunia, na tunajenga upya nyumba iliyojengwa miaka mingi iliyoipita, ambayo mfalme fulani mkuu wa Israeli alijenga na kukamilisha.’^b

12 Lakini kwa sababu baba zetu walimkasirisha Mungu wa mbinguni,^c aliwatia mikononi mwa Mfalme Nebukadneza^d wa Babiloni, Mkaldayo, ambaye aliibomoa nyumba hii^e na kuwapeleka watu uhamishoni huko Babiloni.^f **13** Hata hivyo, katika mwa-

5:8; 6:2 *Au “wilaya ya utawala.” 5:9 *Au “mihimili hii.”

SURA YA 5

a Ezr 5:3, 4

b 1Fa 7:51

c Kum 31:17
2Nya 34:24, 25

d 2Fa 24:1
2Fa 25:1

e 2Fa 25:8, 9

f 2Fa 25:11

Safu ya 2

a Ezr 1:1-3

b 2Fa 25:14, 15
2Nya 36:7, 18

c Ezr 1:8, 11

d Hag 1:1, 14

e Ezr 1:2, 7

f Ezr 3:10
Hag 2:18
Zek 4:9

g Ezr 4:23, 24

h 2Nya 36:22, 23
Ezr 6:3, 4

ka wa kwanza wa utawala wa Mfalme Koreshi wa Babiloni, Mfalme Koreshi alitoa agizo la kuijenga upya nyumba hii ya Mungu.^a **14** Pia, Mfalme Koreshi alitoa katika hekalu la Babiloni vyombo vya dhahabu na fedha vya nyumba ya Mungu ambavyo Nebukadneza alikuwa amevichukua hekaluni huko Yerusalemu, na kuvileta katika hekalu la Babiloni.^b Alivikabidhi kwa mtu aitwaye Sheshbazari,^{*c} ambaye Koreshi alimteua kuwa gavana.^d **15** Koreshi alimwambia: “Chukua vyombo hivi, uvirudishe katika hekalu lililo Yerusalemu, na nyumba ya Mungu ijengwe upya mahali ilipokuwa awali.”^e **16** Ndipo Sheshbazari akaja, akaweka misingi ya nyumba ya Mungu,^f iliyo Yerusalemu; na tangu wakati huo mpaka leo inaendelea kujengwa lakini haijamaliza.^g

17 “Basi mfalme ukipenda, acha uchunguzi ufanywe katika nyumba ya hazina ya mfalme iliyo Babiloni, ili ijulikane kama Mfalme Koreshi alitoa agizo la kuijenga upya nyumba ya Mungu huko Yerusalemu;^h kisha wewe mfalme ututumie uamuzi wako kuhusu jambo hili.”

6 Ndipo Mfalme Dario akatoa agizo, nao wakafanya uchunguzi katika jengo la hifadhi* ambamo hazina ziliwekwa huko Babiloni. **2** Kisha kitabu cha kukunjwa kikapatikana kwenye ngome huko Ekibatana,^g katika mkoa* wa

5:14 *Labda ni Zerubabeli anayetajwa kwenye Ezr 2:2; 3:8. 6:1 *Tnn., “nyumba ya kumbukumbu.”

Umedi, nacho kilikuwa na ujumbe ufuatao:

3 “Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Mfalme Koreshi, Mfalme Koreshi alitoa agizo hili kuhusu nyumba ya Mungu huko Yerusalemu:^a ‘Nyumba hiyo na ijengwe upya iwe mahali watakapotelea dhabihu, na misingi yake inapaswa kuwekwa; kimo chake kiwe mikono 60,^{*} upana wake mikono 60,^b **4** na iwe na safu tatu za mawe makubwa yaliyobingirishwa na kuwekwa mahali pake na safu moja ya mbao;^c na gharama zote zilipwe kutoka katika nyumba ya mfalme.^d **5** Pia, vyombo vya dhahabu na fedha vya nyumba ya Mungu ambavyo Nebukadneza alivichukua katika hekalu lililokuwa Yerusalemu na kuvileta Babiloni^e virudishwe, ili viwekwe mahali pake katika hekalu huko Yerusalemu na vihifadhiwe katika nyumba ya Mungu.’^f

6 “Basi, Tatenai gavana wa eneo lililo Ng’ambo ya Mto,^{*} Shethar-bozenai, na wenzenu, magavana wadogo wa eneo lililo Ng’ambo ya Mto^g—msikaribie mahali hapo. **7** Msiingilie kazi ya nyumba hiyo ya Mungu. Gavana wa Wayahudi na wazee wa Wayahudi watajenga upya nyumba hiyo ya Mungu mahali ilipokuwa zamani. **8** Pia, ninatoa agizo kuhusu jambo mnalopaswa kuwafanyia wazee hao wa Wayahudi kwa ajili ya kujenga upya nyumba hiyo ya Mungu: Gharama zao zote zitalipwa bila kuchelewa kutoka katika hazina ya

6:3 *Karibu mita 26.7 (futi 87.6). Angalia Nyongeza B14. 6:6 *Au “maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati.”

SURA YA 6

a 2Nya 36:22, 23
Ezr 1:1-3

b 1Fa 6:2

c Ezr 3:7
Ezr 5:8

d Ezr 7:20
Isa 49:23

e 2Fa 25:13-15
2Nya 36:7, 18
Da 1:1, 2
Da 5:2

f Ezr 1:8, 11

g Ezr 5:3, 6

Safu ya 2

a Ezr 7:20
Hag 2:7, 8

b Ezr 5:5

c Law 1:3, 5

d Law 1:10

e Hes 28:3

f Law 2:1

g Law 2:13

h Hes 15:5

i Kut 27:20
Law 2:4

j Ezr 7:23

k Kum 12:5, 6
2Nya 7:16

l Ezr 5:6

m Ezr 3:8
Ezr 4:3

n Hag 1:12

o Ezr 5:1, 2
Zek 1:1, 7
Zek 6:15

mfalme,^a kodi inayokusanywa katika eneo lililo Ng’ambo ya Mto, ili ujenzi uendelee bila kukatizwa.^b **9** Na chote kinachohitajiwa—ng’ombe dume wachanga^c pamoja na kondoo dume^d na wanakondoo^e kwa ajili ya dhabihu za kuteketezwa kwa Mungu wa mbinguni, ngano,^f chumvi,^g divai,^h na mafuta,ⁱ kama watakavyosema makuhani walio Yerusalemu—waendeleo kupeva vitu hivyo siku baada ya siku bila kukosa, **10** ili waendeleo kutoa matoleo yanayompendeza Mungu wa mbinguni na kumwomba mfalme na wanawe wawe na maisha marefu.^j **11** Pia nimetoa agizo kwamba yeyote atakayevunja amri hii, nguzo itang’olewa katika nyumba yake naye atatundikwa juu ya nguzo hiyo, na nyumba yake itafanywa kuwa choo cha umma^{*} kwa sababu ya kosa hilo. **12** Na Mungu aliyefanya jina lake likae huko^k na ampindue mfalme yeyote na watu watakaonyoosha mkono ili kukiuka agizo hili na kuiharibu nyumba ya Mungu, iliyo Yerusalemu. Mimi, Dario, ninatoa agizo hili. Nalo litekelezwe bila kukawia.”

13 Ndipo Tatenai gavana wa eneo lililo Ng’ambo ya Mto, Shethar-bozenai,^l na wenzao, wakatekeleza bila kukawia kila jambo ambalo Mfalme Dario alikuwa ameagiza. **14** Nao wazee wa Wayahudi wakaendelea kujenga na kufanya maendeleo,^m wakitiwa moyo na nabii Hagaiⁿ na Zekaria^o mjukuu wa Ido; wakamali-

6:11 *Au labda, “eneo la takataka; rundo la mavi.”

za kujenga kulingana na agizo la Mungu wa Israeli^a na agizo la Koreshi,^b Dario,^c na Mfalme Artashasta^d wa Uajemi. **15** Wakamaliza kujenga nyumba hiyo katika siku ya tatu wa mwezi wa Adari,* katika mwaka wa sita wa utawala wa Mfalme Dario.

16 Ndipo Waisraeli, makuhani, Walawi,^e na watu wengine waliotoka uhamishoni wakaizindua* nyumba ya Mungu kwa shangwe. **17** Nao wakaleta kwa ajili ya kuzindua nyumba ya Mungu ng'ombe dume 100, kondoo dume 200, wanakondoo 400, na mbuzi dume 12 kuwa dhabihu ya dhambi kwa ajili ya Waisraeli wote, kulingana na idadi ya makabila ya Israeli.^f **18** Nao wakawapanga makuhani katika makundi yao na Walawi katika vikundi vyao kwa ajili ya utumishi wa Mungu huko Yerusalemu,^g kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Musa.^h

19 Na watu hao waliotoka uhamishoni wakasherehekea Pasaka siku ya 14 ya mwezi wa kwanza.ⁱ **20** Makuhani na Walawi wote, walikuwa wamejitakasa,^j hivyo wote walikuwa safi; basi wakachinja mnyama wa Pasaka kwa ajili ya watu wote waliotoka uhamishoni, kwa ajili ya makuhani wenzao, na kwa ajili yao wenyewe. **21** Kisha Waisraeli waliorudi kutoka uhamishoni wakala pamoja na kila mtu aliyekuwa amejiunga nao na kujitenga na uchafu wa mataifa ya nchi hiyo ili kumwabudu* Yehova Mungu wa Israeli.^k

6:15 *Angalia Nyongeza B15. 6:16 *Au "wakaiweka wakfu." 6:21 *Tnn., "kumtafuta."

SURA YA 6

a Hag 1:8

b 2Nya 36:23
Ezr 1:2, 3
Isa 44:28

c Ezr 6:12

d Ezr 7:12, 13

e 1Nya 9:2
Ne 7:73

f 2Nya 7:5

g 1Nya 23:6

h Hes 3:6

i Kut 12:2, 14
Law 23:5
Kum 16:1
Est 3:7j Kut 30:19, 20
Law 21:8
Law 22:2, 3k Kut 12:48
Hes 9:14

Safu ya 2

a Kut 12:17
Law 23:6b Ezr 7:27
Met 21:1

SURA YA 7

c Ne 2:1

d Ne 8:2
Ne 12:26

e 1Nya 6:14

f 2Fa 22:8

g 2Nya 31:10

h Hes 25:11
Amu 20:28i Kut 6:23, 25
Hes 3:32
Kum 10:6j Kut 7:1
Kut 28:1

k Ne 8:1, 4

l Ezr 8:18, 19

m 1Nya 6:31, 32

n 1Nya 9:22-27

o 1Nya 9:2
Ezr 8:20

22 Pia, wakasherehekea kwa shangwe Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu^a kwa siku saba, kwa maana Yehova aliwafanya washangilie na alikuwa ameugeza moyo wa mfalme wa Ashuru ili awatendee mema,^b hivi kwamba akawaunga mkono* katika kazi ya nyumba ya Mungu wa kweli, Mungu wa Israeli.

7 Baada ya mambo hayo, wakati wa utawala wa Mfalme Artashasta^c wa Uajemi, Ezra^{*d} akarudi. Alikuwa mwana wa Seraya,^e mwana wa Azaria, mwana wa Hilkia,^f **2** mwana wa Shalumu, mwana wa Sadoki, mwana wa Ahitubu, **3** mwana wa Amaria, mwana wa Azaria,^g mwana wa Merayothi, **4** mwana wa Zeraya, mwana wa Uzi, mwana wa Buki, **5** mwana wa Abishua, mwana wa Finehasi,^h mwana wa Eleazari,ⁱ mwana wa kuhani mkuu Haruni.^j **6** Huyo Ezra alitoka Babiloni. Alikuwa mwandishi* na alijiua vizuri[#] Sheria ya Musa,^k iliyotolewa na Yehova Mungu wa Israeli. Mfalme alimpa kila kitu alichoomba, kwa maana mkono wa Yehova Mungu wake ulikuwa juu yake.

7 Baadhi ya Waisraeli, makuhani, Walawi,^l waimbaji,^m walinzi wa malango,ⁿ na watumishi wa hekaluni,^{*o} wakapanda kwenda Yerusalemu katika mwaka wa saba wa utawala wa Mfalme Artashasta. **8** Naye Ezra akaja Yerusalemu mwezi wa

6:22 *Tnn., "akaitia nguvu mikono yao." 7:1 *Maana yake "Msaada." 7:6 *Au "Alinakili maandishi." #Au "Alikuwa mwandishi stadi wa." 7:7 *Au "Wanethini." Tnn., "waliotolewa."

tano, katika mwaka wa saba wa utawala wa mfalme huyo. **9** Alianza safari ya kutoka Babiloni siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza, akafika Yerusalemu siku ya kwanza ya mwezi wa tano, kwa sababu mkono mwema wa Mungu wake ulikuwa juu yake.^a **10** Ezra alikuwa ameutayari-sha moyo wake* kuichunguza Sheria ya Yehova na kui-fuata,^b na kufundisha masharti ya sheria hiyo na maamuzi yake katika Israeli.^c

11 Ifuatayo ni nakala ya barua ambayo Mfalme Artashasta alimpa Ezra aliyekuwa kuhani na mwandishi,* mwenye ujuzi mwingi[#] kuhusu amri za Yehova na masharti aliyowapa Waisraeli:

12 * "Artashasta,^d mfalme wa wafalme, kwa kuhani Ezra, mwandishi[#] wa Sheria ya Mungu wa mbinguni: Na uwe na amani kamili. Na sasa **13** nimetoa agizo kwamba kila mtu katika milki yangu ambaye ni mmoja wa watu wa Israeli na pia makuhani wao na Walawi, ambaye angependa kwenenda nawe Yerusalemu aende.^e **14** Kwa maana umetumwa na mfalme na washauri wake saba ili kuchunguza kama watu walio Yuda na Yerusalemu wanafuata Sheria ya Mungu wako uliyo nayo,* **15** na kuchukua fedha na dhahabu ambayo mfalme na washauri wake wamemtolea kwa hia-

7:10 *Au "alikuwa ameamuzia moyoni mwake." 7:11 *Au "mtu aliyenakili maandishi." *Au "aliyenakili maneno." 7:12 *Mwanzoni, maandishi ya Ezr 7:12 hadi 7:26 yaliandikwa katika Kiaramu. *Au "aliyenakili maandishi." 7:14 *Tnn., "iliyo mkononi mwako."

SURA YA 7

a Ezr 8:22

b Kum 5:1
Kum 17:10c Kum 33:8, 10
Mal 2:7d Ezr 6:14
Ne 2:1

e Ezr 1:2, 3

Safu ya 2

a Ezr 1:5, 6
Ezr 8:25

b Law 1:3

c Law 1:10

d Hes 28:3

e Hes 15:4

f Hes 15:5

g Ezr 8:30

h Ezr 6:3, 4
Ezr 6:8i Ezr 7:6
Ne 8:2

ri Mungu wa Israeli, ambaye makao yake yako Yerusalemu, **16** pamoja na fedha na dhahabu yote ambayo utapokea* katika mkoa wote[#] wa Babiloni, na pia zawadi ambazo watu na makuhani hutoa kwa hiari kwa ajili ya nyumba ya Mungu wao iliyo Yerusalemu.^a **17** Na bila kukawia utanunua kwa pesa hizo ng'ombe dume,^b kondoo dume,^c wanakondoo,^d na matoleo yao ya nafaka^e na matoleo yao ya kinywaji,^f nawe utavitao juu ya madhabahu ya nyumba ya Mungu wenu huko Yerusalemu.

18 "Na fedha na dhahabu itakayobaki, wewe na ndugu zako mnaweza kuitumia mtakavyopenda, kulingana na mapenzi ya Mungu wenu. **19** Na vyombo vyote utakavyopewa kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya Mungu wako, unapaswa kuvipeleka mbele za Mungu huko Yerusalemu.^g **20** Na kitu kingine chochoite unachohitaji kutoa kwa ajili ya nyumba ya Mungu wako, utakitoe kutoka katika hazina ya mfalme.^h

21 "Mimi, Mfalme Artashasta, nimewaagiza wawekahazina wote katika eneo lililo Ng'ambo ya Mto* wampe bila kukawia kila kitu atakachomba Ezra,ⁱ kuhani na mwandishi wa[#] Sheria ya Mungu wa mbinguni, **22** hata akiomba talanta 100 za fedha,* kori 100

7:16 *Tnn., "utapata." *Au, "wilaya yote ya utawala." 7:21 *Au "maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati." *Au "aliyenakili maandishi ya." 7:22 *Talanta ilikuwa sawa na kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14.

za ngano,* bathi 100 za divai,^{#a} bathi 100 za mafuta,^b na chumvi isiyo na kipimo.^c

23 Kila jambo ambalo Mungu wa mbinguni ameagiza linapaswa kufanywa kwa bidii kwa ajili ya nyumba ya Mungu wa mbinguni,^d ili ghadhabu yake isije dhidi ya milki yangu na wanangu.^e **24** Pia ninawajulisha kwamba hairuhusiwi kuwatoza kodi, wala ushuru,^f wala ada yoyote makuhani na Walawi, wanamuziki,^g walinzi wa malango, watumishi wa hekaluni,^{*h} na wafanyakazi wa nyumba hii ya Mungu.

25 “Na wewe, Ezra, kulingana na hekima uliyopewa na Mungu wako,* teua mahakimu na waamuzi ili wawahukumu watu wote katika eneo lililo Ng’ambo ya Mto, wote wanaojua sheria za Mungu wako; nanyi mnapaswa kumfundisha yeyote asiyezijua.ⁱ **26** Na kila mtu ambaye hatafuata Sheria ya Mungu wako na sheria ya mfalme anapaswa kuhukumiwa upesi, iwe ni kuuawa, kufukuzwa nchini, kutozwa faini, au kufungwa gereza.”

27 Yehova Mungu wa mababu zetu na asifiwe, ambaye alitia ndani ya moyo wa mfalme wazo la kuipamba nyumba ya Yehova iliyo Yerusalemu! **28** Naye amenitendea kwa upendo mshikamanifu mbele ya mfalme,^k washauri wake,^l na wakuu wote wa mfalme we-

7:22 *Kori moja ilikuwa sawa na lita 220 (kilogramu 170 hivi). Angalia Nyongeza B14. [#]Bathi ilikuwa sawa na lita 22. Angalia Nyongeza B14. 7:24 *Au “Wanethini.” Tnn., “waliotolewa.” 7:25 *Tnn., “kulingana na hekima ya Mungu wako iliyo mkononi mwako.”

SURA YA 7

a Hes 15:5

b Kut 27:20
Law 2:1

c Law 2:13

d Ezr 1:2

e Ezr 6:9, 10

f Ne 5:4

g 1Nya 15:16

h 1Nya 9:2

i Ne 8:2, 3

j Ezr 6:22
Met 21:1
Isa 60:13k Ezr 9:9
Ne 1:11

l Ezr 7:14

Safu ya 2

SURA YA 8

a Ezr 7:7

b 1Nya 6:3, 4

c Kut 6:23

d Ezr 2:1, 6

e Ezr 2:1, 8
Ezr 10:27, 44

f Ezr 2:1, 15

g Ezr 2:1, 7

h Ezr 2:1, 4

i Ezr 2:1, 11
Ezr 10:28, 44

nye nguvu. Hivyo nikajipa ujasiri* kwa sababu mkono wa Yehova Mungu ulikuwa juu yangu, nami nikawakusanya wanaume waliokuwa viongozi[#] katika Israeli ili wapande pamoja nami.

8 Basi hawa ndio waliokuwa viongozi wa koo* na hii ndiyo orodha ya ukoo wa wale waliopanda pamoja nami kutoka Babiloni wakati wa utawala wa Mfalme Artashasta:^a **2** ukoo wa wana wa Finehasi,^b Gershomu; wa wana wa Ithamari,^c Danieli; wa wana wa Daudi, Hatushi; **3** wa wana wa Shekania, wa wana wa Paroshi, Zekaria, na pamoja naye kulikuwa na wanaume 150 walioandikishwa; **4** wa wana wa Pahathmoabu,^d Elieho-enai mwana wa Zeraya, na wanaume 200 pamoja naye; **5** wa wana wa Zatu,^e Shekania mwana wa Yahazieli, na wanaume 300 pamoja naye; **6** wa wana wa Adini,^f Ebedi mwana wa Yonathani, na wanaume 50 pamoja naye; **7** wa wana wa Elamu,^g Yeshaya mwana wa Athalia, na wanaume 70 pamoja naye; **8** wa wana wa Shefatia,^h Zebadia mwana wa Mikaeli, na wanaume 80 pamoja naye; **9** wa wana wa Yoabu, Obadia mwana wa Yehieli, na wanaume 218 pamoja naye; **10** wa wana wa Bani, Shelomithi mwana wa Yosifia, na wanaume 160 pamoja naye; **11** wa wana wa Bebai, Zekaria mwana wa Bebai, na wanaume 28 pamoja naye;

7:28 *Au “nikajipa nguvu.” [#]Tnn., “vichwa.” **8:1** *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

12 wa wana wa Azgadi,^a Yohanani mwana wa Hakatani, na wanaume 110 pamoja naye; **13** wa wana wa Adonikamu,^b wale waliokuwa wa mwisho, haya ndiyo majina yao: Elifeleti, Yeieli, na Shemaya, na wanaume 60 pamoja nao; **14** na wa wana wa Bigvai,^c Uthai na Zabudu, na wanaume 70 pamoja nao.

15 Nikawakusanya kwenye mto unaoelekea Ahava;^d nasi tukapiga kambi hapo siku tatu. Lakini nilipowakagua watu na makuhani, sikupata Mlawi hata mmoja. **16** Kwa hiyo nikawatuma wajumbe wawaite Eliezeri, Arieli, Shemaya, Elnathani, Yariibu, Elnathani, Nathani, Zekaria, na Meshulamu, waliokuwa viongozi, na Yoyaribu na Elnathani, waliokuwa walimu. **17** Kisha nikawapa amri kuhusu Ido kiongozi wa Kasifia. Nikawaagiza wamwambie Ido na ndugu zake, watumishi wa hekaluni* waliokuwa huko Kasifia, watulettee wahudumu kwa ajili ya nyumba ya Mungu wetu. **18** Kwa kuwa mkono mwema wa Mungu wetu ulikuwa juu yetu, walituletea mwanamume mwenye busara kutoka kwa wana wa Mali^e mjukuu wa Lawi mwana wa Israeli, aliyeitwa Sherebia,^f na wanawe na ndugu zake, wanaume 18; **19** na Hashabia, na pamoja naye Yeshaya kutoka kwa Wamerari,^g ndugu zake na wana wao, wanaume 20. **20** Na kulikuwa na watumishi wa hekaluni* 220, ambao Daudi na wakuu walikuwa wamewatoa

8:17, 20 *Au "Wanethini." Tnn., "waliolelewa."

SURA YA 8

a Ezr 2:1, 12

b Ne 7:6, 18

c Ezr 2:1, 14

d Ezr 8:31

e Hes 3:20

f Ezr 8:24, 25

g 1Nya 6:16

Safu ya 2

a 2Nya 16:9

Ezr 7:6

Ezr 7:28

Zek 4:6

b 2Nya 15:2

c 2Nya 7:14
Yer 29:10, 12
Yer 50:4, 5

d Ezr 8:18, 19

e Ezr 7:14-16
Ezr 7:19

kwa ajili ya utumishi wa Wala-wi, wote walikuwa wametajwa kwa majina.

21 Kisha nikatangaza kwa mba watu wafunge hapo kwenye mto Ahava, ili tujinyenyekeze mbele za Mungu wetu, na kumwomba atuongoze katika safari yetu, sisi na watoto wetu na mali zetu zote.

22 Niliona aibu kumwomba mfalme wanajeshi na wapanda farasi watulinde dhidi ya maadui njiani, kwa sababu tulikuwa tumemwambia mfalme: "Mkono mwema wa Mungu wetu uko juu ya wale wote wanaomtafuta,^a lakini nguvu zake na hasira yake iko dhidi ya wote wanaomwacha."^b

23 Basi tukafunga na kumwomba Mungu wetu kuhusu jambo hilo, naye akasiliza maombi yetu.^c

24 Kisha nikachagua wakuu 12 wa makuhani, yaani, Sherebia na Hashabia,^d pamoja na kumi kati ya ndugu zao. **25** Nikawapimia fedha na dhahabu na vyombo, mchango ambao mfalme na washauri wake na wakuu wake na Waisraeli wote waliokuwa hapo walitoa kwa ajili ya nyumba ya Mungu wetu.^e

26 Basi nikapima na kuwaka-bidhi talanta 650 za fedha,* vyombo 100 vya fedha vyenye thamani ya talanta mbili, na talanta 100 za dhahabu, **27** mabakuli madogo 20 ya dhahabu yenye thamani ya dariki 1,000,* na vyombo viwili vya shaba bora, nyeku-

8:26 *Talanta ilikuwa sawa na kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. 8:27 *Dariki ilikuwa sarafu ya dhahabu ya Waajemi. Angalia Nyongeza B14.

ndu inayong'aa, inayotamani-ka kama dhahabu.

28 Kisha nikawaambia: "Ninyi ni watakatifu kwa Yehova,^a na vyombo hivi ni vitakatifu, na fedha na dhahabu hii ni matoleo ya hiari kwa Yehova Mungu wa mababu zenu. **29** Mvilinde kwa makini hadi mtakapovipima mbele ya wakuu wa makuhani na Walawi na wakuu wa koo za Waisraeli huko Yerusalemu,^b katika vyumba vya* nyumba ya Yehova." **30** Makuhani na Walawi wakapokea fedha na dhahabu na vyombo walivyo-pimiwa, ili wavilete Yerusalemu kwenye nyumba ya Mungu wetu.

31 Mwishowe tukaondoka kwenye mto Ahava^c siku ya 12 ya mwezi wa kwanza^d na kuelekea Yerusalemu, na mkono wa Mungu wetu ulikuwa juu yetu, naye akatuokoa kutoka mikononi mwa maadui na wavamizi njiani. **32** Basi tukafika Yerusalemu^e na kukaa huko siku tatu. **33** Kisha siku ya nne tukapima ile fedha na dhahabu na vyombo katika nyumba ya Mungu wetu,^f tukamkabidhi Meremothi^g mwana wa kuhani Uriya, aliyekuwa pamoja na Eleazari mwana wa Finehasi, pamoja na Walawi Yozabadi^h mwana wa Yeshua na Nodia mwana wa Binui.ⁱ **34** Kila kitu kilihesabiwa na kupimwa, na uzito wote ukaandikwa. **35** Wale walio-toka uhamishoni, waliokuwa utekwani, wakamtolea Mungu wa Israeli dhabihu za kuteke-
tezwa, ng'ombe dume 12^j kwa

8:29 *Au "majumba ya kulia chakula ya."

SURA YA 8

a Law 21:6-8
Isa 52:11

b Ezr 7:19
Ezr 8:33

c Ezr 8:15, 21

d Est 3:7

e Ezr 7:8

f Ezr 7:19
Ezr 8:29

g Ne 3:4, 21

h Ne 8:7

i Ne 12:1, 8

j Law 1:3

Safu ya 2

a Law 1:10

b Law 22:18, 19

c Ezr 7:17

d Ezr 7:21

e Mwa 15:18

f Ezr 6:13

SURA YA 9

g Law 20:23
Kum 12:29, 30

h Law 18:3

i Mwa 15:16

j Kut 34:15, 16
Ezr 10:44

k Kut 19:5, 6

l Ne 13:1, 3

ajili ya Waisraeli wote, kondoo dume 96,^a wanakondoo dume 77, mbuzi dume 12^b kwa ajili ya dhabihu ya dhambi; hizo zote zilikuwa dhabihu za kuteke-
tezwa zilizotolewa kwa Yehova.^c

36 Kisha tukawapa maliwali* wa mfalme^d na magavana waliokuwa Ng'ambo ya Mto^e maagizo ya mfalme, nao wakawategemeza watu na nyumba ya Mungu wa kweli.^f

9 Baada ya mambo hayo kufanywa, wakuu wakaja na kuniambia: "Watu wa Israeli na makuhani na Walawi hawajaitenga na watu wa mataifa ya nchi mbalimbali na mazoea yao yanayochukiza,^g ya Wakanaani, Wahiti, Wape-rizi, Wayebusi, Waamoni, Wa-moabu, Wamisri,^h na Waamori.ⁱ **2** Wamejichukulia baadhi ya mabinti wa mataifa hayo kuwa wake zao na kuwachukulia wana wao pia.^j Sasa wao, uzao mtakatifu,^{*k} wamechanganyika na watu wa mataifa ya nchi mbalimbali.^l Wakuu na watawala wasaidizi ndio wanaoongoza katika ukosefu huu wa uaminifu."

3 Mara tu niliposikia jambo hilo, nikalirarua vazi langu na joho langu lisilo na mikono na kung'oa baadhi ya nywele za kichwa changu na ndevu zangu, nami nikaketi chini kwa mshtuko. **4** Kisha kila mtu aliyehofu* maneno ya Mungu wa Israeli akakusanyika kunizunguka

8:36 *Cheo kinachomaanisha "walinzi wa milki," hapa cheo hicho kinawahusu magavana wa mikoa ya Milki ya Uajemi. ^aAu "maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati." 9:2 *Tnn., "mbegu takatifu." 9:4 *Tnn., "aliyetetemeka kwa sababu ya."

kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu wa watu waliotoka uhamishoni, nami nilikuwa nimeketi chini kwa mshtuko mpaka wakati wa toleo la nafa-ka la jioni.^a

5 Wakati wa toleo la nafa-ka la jioni,^b niliinuka kuto-ka mahali nilipokuwa nimeketi kwa aibu, vazi langu na joho langu lisilo na mikono likiwa limeraruka, nikapiga magoti na kumnyooshea mikono Yehova Mungu wangu. **6** Nikasema: “Ee Mungu wangu, ninaona aibu na haya kuuinua uso wangu kwako, Ee Mungu wangu, kwa sababu makosa yetu yameongezeka juu ya vichwa vyetu na hatia yetu ime-rundamana mpaka mbinguni.^c **7** Tangu siku za mababu zetu mpaka leo hii tumekuwa na hatia kubwa;^d na kwa sababu ya makosa yetu, sisi, wafalme wetu, na makuhani wetu, tumetiwa mikononi mwa wafalme wa nchi nyingine, tumeuawa kwa upanga,^e tumepeleka utekwani,^f tumeporwa,^g tumetiwa aibu, kama ilivyo leo.^h **8** Lakini sasa kwa muda mfupi, Yehova Mungu wetu ametuonyesha kibali kwa kuruhusu baadhi yetu tuponyoke na kutupatia sehemu salama* mahali pake patakati-fu,ⁱ ili kuyafanya macho yetu yang’ae, Ee Mungu wetu, na kutupumzisha kidogo kutoka katika utumwa wetu. **9** Inga-wa sisi ni watumwa,^j Mungu wetu hajatuacha utumwani; bali ametutendea kwa upe-ndo mshikamanifu mbele ya wafalme wa Uajemi,^k ili kutu-pumzisha tuweze kuisimami-sha nyumba ya Mungu wetu!

9:8 *Tnn., “kigingi.”

SURA YA 9

a Kut 29:41

b Hes 28:4, 5

c Da 9:7

d Hes 32:14
2Nya 29:6e 2Fa 10:32
2Nya 36:17f 2Fa 17:22, 23
2Fa 25:6, 7

g 2Fa 17:20

h Ne 9:32

i Ne 9:31
Zb 138:7

j Ne 9:36, 37

k Ezr 1:1-3

l Ezr 6:14
Zek 4:9

Safu ya 2

a Law 18:24
Kum 12:30, 31
Kum 18:9-11b Kut 23:32
Kut 34:15, 16
Kum 7:3, 4
Yos 23:12, 13

c Kum 23:3, 6

d Zb 103:8, 10
Omb 3:22

e Zb 106:46

f Ezr 9:1
Ne 13:23g Ne 9:33
Da 9:7

na kuijenga upya nyumba hiyo ambayo ni magofu na kutu-patia ukuta wa mawe* katika Yuda na Yerusalemu.

10 “Lakini tuseme nini sasa, Ee Mungu wetu, baada ya hayo? Kwa maana tumeziacha amri zako, **11** ulizotupatia kupitia watumishi wako manabii, ukisema: ‘Nchi ambayo mnaingia kuimiliki ni nchi chafu kwa kuwa watu waliomo ni wachafu, kwa sababu ya matendo yao yanayochukiza ambayo wameyajaza kutoka mwisho mmoja hadi mwingine kwa uchafu wao.’ **12** Kwa hiyo, msiwaruhusu mabinti zenu waolewe na wana wao, wala msikubali wana wenu wawaoe mabinti zao;^b msiwatakie kamwe amani wala mafanikio,^c ili mzidi kupata nguvu na kula mema ya nchi na kuimiliki ili wana wenu wairithi milele.’ **13** Baada ya yote yaliyotupata kwa sababu ya matendo yetu maovu na hatia yetu kubwa—kwa maana wewe, Ee Mungu wetu, hujatutendea kulingana na makosa yetu,^d nawe umeruhusu sisi tulio hapa tuponyoke— **14** je, tuvunje tena amri zako na kufanya mapatano ya ndoa* na watu wanaotenda mambo haya yanayochukiza?^f Je, hutatukasiria vikali na kutuangamiza kabisa, hata kusiwe na yeyote atakayebaki wala kuokoka? **15** Ee Yehova Mungu wa Israeli, wewe ni mwadilifu,^g kwa maana tumeokoka na kubaki mpaka leo. Sasa tumesi-

9:9 *Au “ukuta wa ulinzi.” 9:14 *Au “na kuoana.”

mama mbele zako tukiwa na hatia, kwa maana hatuwezi kusimama mbele zako kwa sababu ya jambo hili.”^a

10 Ezra alipokuwa akisali^b na kuungama, aki- lia na kulala kifudufudi mbele ya nyumba ya Mungu wa kweli, umati mkubwa wa wanau- me, wanawake, na watoto wa Israeli wakakusanyika kumzu- nguka, kwa maana watu wa- likuwa wakilia sana. **2** Ndi- po Shekania mwana wa Yehi- eli^c wa wana wa Elamu^d aka- mwambia Ezra: “Tumetenda kwa ukosefu wa uaminifu dhi- di ya Mungu wetu kwa kuoa* wanawake wa kigeni kutoka kwa mataifa ya nchi hii.^e Inga- wa hivyo, bado kuna tumai- ni kwa Israeli. **3** Basi na tu- fanye agano na Mungu wetu^f la kuwafukuza wake hao wote na watoto wao kulingana na mwongozo wa Yehova na wa- le wanaohofu* amri ya Mu- ngu wetu.^g Na tutende kuli- ngana na Sheria. **4** Simama, kwa maana jambo hili ni ju- kumu lako, nasi tuko pamoja nawe. Uwe imara na uchukue hatua.”

5 Ndipo Ezra akasimama, akawaapisha wakuu wa ma- kuhani, Walawi, na Wais- raeli wote kwamba watafa- nya kama ilivyosemwa.^h Basi wakaapa. **6** Sasa Ezra akaon- doka mbele ya nyumba ya Mungu wa kweli na kwenda katika chumba cha* Yehoha- nani mwana wa Eliashibu. Ingawa alienda huko, haku- la chakula wala kunywa maji,

10:2 *Au “kwa kuwaingiza ndani ya nyu- mba zetu.” 10:3 *Tnn., “wanaotetemeka.” 10:6 *Au “jumba la kulia cha- kula la.”

SURA YA 9

a Zb 130:3
Zb 143:2

SURA YA 10

b Ezr 9:5, 6

c Ezr 10:26, 44

d Ezr 2:1, 7

e Ezr 9:2

f 2Fa 11:17
2Nya 29:10
2Nya 34:31

g Ezr 9:4

h Ne 10:28-30

Safu ya 2

a Ezr 9:3, 4
Da 9:3-5

b Ezr 7:26

c Ne 13:23

d Kum 7:3, 4
Ne 13:3
2Ko 6:17

kwa maana alikuwa akiombo- leza kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu wa watu walioto- ka uhamishoni.^a

7 Ndipo wakatangaza kote- kote katika Yuda na Yerusale- mu kwamba watu wote walio- toka uhamishoni wakusanyike Yerusalemu; **8** na wakuu na wanaume wazee wakaamua kwamba yeyote ambaye ha- ngekuja katika muda wa siku tatu, mali zake zote zingechu- kuliwa,* naye angefukuzwa kutoka kwenye kutaniko la watu waliotoka uhamisho- ni.^b **9** Basi wanaume wote wa Yuda na Benjamini waka- kusanyika Yerusalemu katika muda wa siku tatu, yaani, ka- tika mwezi wa tisa siku ya 20 ya mwezi huo. Watu wote wa- likuwa wameketi kwenye uwa- nja wa nyumba ya Mungu wa kweli, wakitetemeka kwa sa- babu ya jambo hilo na kwa sa- babu ya mvua kubwa.

10 Kisha kuhani Ezra akasi- mama na kuwaambia: “Mmete- nda kwa ukosefu wa uaminifu kwa kuoa wanawake wa kige- ni^c na hivyo mmeongeza hatia ya Israeli. **11** Sasa ungame- ni kwa Yehova Mungu wa ma- babu zenu na mfanye mape- nzi yake. Jitengeni na watu wa mataifa na hawa wake wa kigeni.”^d **12** Ndipo kutaniko lote likajibu hivi kwa sauti kubwa: “Ni wajibu wetu kufa- nya kikamili mambo unayotua- mbia. **13** Hata hivyo, watu ni wengi, na haya ni majira ya mvua. Haiwezekani kusimama nje, na jambo hili halitama- lizika kwa siku moja au mbi- li, kwa maana tumeasi sana katika jambo hili. **14** Basi,

10:8 *Au “zingezuiliwa.”

tafadhali, acha wakuu wetu waliwakilishe kutaniko lote;^a na watu wote katika majiji yetu ambao wameoa wanawake wa kigeni waje wakati uliowekwa, pamoja na wazee na waamuzi wa kila jiji, mpaka tutakapoituliza hasira inayowaka ya Mungu wetu kuhusiana na jambo hili.”

15 Hata hivyo, Yonathani mwana wa Asaheli na Yahzeya mwana wa Tikva wakapinga jambo hilo, na Meshulamu na Shabethai, waliokuwa Walawi,^b wakawauunga mkono. **16** Lakini watu waliotoka uhamishoni wakafanya kama ilivyokubaliwa; na kuhani Ezra na viongozi wa koo,* watu wote ambao majina yao yalikuwa yameorodheshwa, wakakusanyika peke yao siku ya kwanza ya mwezi wa kumi ili kuchunguza jambo hilo; **17** na kufikia siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza wakamaliza kuwachunguza wanaume wote waliokuwa wameoa wanawake wa kigeni. **18** Na ikagunduliwa kwamba baadhi ya wana wa makuhani walikuwa wameoa wanawake wa kigeni;^c kutoka kwa wana wa Yeshua^d mwana wa Yehosadaki na ndugu zake, Maaseya, Eliezeri, Yarithu, na Gedalia. **19** Lakini wakaahidi* kuwafukuza wake zao, na kwa kuwa walikuwa na hatia, wangetoa kondoo dume wa kundi kwa ajili ya hatia yao.^e

20 Kutoka kwa wana wa Imeri,^f kulikuwa na Hanani na Zebadia; **21** na kutoka kwa wana wa Harimu,^g Maa-

SURA YA 10

a Ezr 9:1

b Ne 8:7
Ne 11:16c Ezr 9:1, 2
Ne 13:28
Eze 44:22
Mal 2:7, 8d Ezr 2:1, 2
Ezr 3:2
Zek 6:11

e Law 5:17, 18

f 1Nya 24:3, 14
Ezr 2:1, 37g 1Nya 24:3, 8
Ezr 2:1, 39

Safu ya 2

a Ezr 2:1, 38

b Ezr 2:1, 3
Ne 3:25c Ezr 2:1, 7
Ezr 8:1, 7

d Ezr 10:2

e Ezr 2:1, 8

f Ezr 2:1, 11
Ezr 8:1, 11

g Ezr 2:1, 6

h Ezr 2:1, 32

i Ne 3:11

j Ezr 2:1, 19
Ne 8:4

seya, Eliya, Shemaya, Yehieli, na Uzia; **22** na kutoka kwa wana wa Pashuri,^a Elioenai, Maaseya, Ishmaeli, Nethaneli, Yozabadi, na Eleasa. **23** Na kutoka kwa Walawi, kulikuwa na Yozabadi, Shimei, Kelaya (yaani, Kelita), Pethahia, Yuda, na Eliezeri; **24** na kutoka kwa waimbaji, Eliashibu; na kutoka kwa walenzi wa malango, Shalumu, Telemu, na Uri.

25 Na kutoka Israeli, kutoka kwa wana wa Paroshi,^b kulikuwa na Ramia, Izia, Malkiya, Miyamini, Eleazari, Malkiya, na Benaya; **26** na kutoka kwa wana wa Elamu,^c Matania, Zekaria, Yehieli,^d Abdi, Yeremothi, na Eliya; **27** na kutoka kwa wana wa Zatu,^e Elioenai, Eliashibu, Matania, Yeremothi, Zabadi, na Aziza; **28** na kutoka kwa wana wa Bebai,^f Yehohanani, Hanania, Zabai, na Athlai; **29** na kutoka kwa wana wa Bani, Meshulamu, Maluku, Adaya, Yashubu, Sheali, na Yeremothi; **30** na kutoka kwa wana wa Pahath-moabu,^g Adna, Kelali, Benaya, Maaseya, Matania, Bezaleli, Binui, na Manase; **31** na kutoka kwa wana wa Harimu,^h Eliezeri, Ishiya, Malkiya,ⁱ Shemaya, Shimeoni, **32** Benjamini, Maluku, na Shemaria; **33** kutoka kwa wana wa Hashumu,^j Matenai, Matata, Zabadi, Elifeleti, Yemai, Manase, na Shimei; **34** kutoka kwa wana wa Bani, Maadai, Amramu, na Ueli, **35** Benaya, Bedeya, Keluhi, **36** Vania, Meremothi, Eliashibu, **37** Matania, Mate-nai, na Yaasu; **38** na kutoka kwa wana wa Binui, Shimei, **39** Shelemia, Natha-

10:16 * Yaani, ukoo wa upande wa baba.
10:19 * Tnn., "walipeana mikono yao ili."

ni, Adaya, **40** Maknadebai, Shashai, Sharai, **41** Azareli, Shelemia, Shemaria, **42** Shalumu, Amaria, na Yosefu; **43** na kutoka kwa wana wa Nebo, Yeieli, Mati-

Safu ya 2

SURA YA 10

a Kum 7:3, 4

b Ezr 10:16, 17

thia, Zabadi, Zebina, Yadai, Yoeli, na Benaya. **44** Wote hao walikuwa wameoa wana-wake wa kigeni,^a basi waka-wafukuza wake zao pamoja na wana wao.^b

NEHEMIA

YALIYOMO

- | | |
|--|---|
| <p>1 Habari kutoka Yerusalemu (1-3)
Sala ya Nehemia (4-11)</p> <p>2 Nehemia aruhusiwa kwenda Yerusalemu (1-10)
Nehemia akagua kuta za jiji (11-20)</p> <p>3 Kuta zajengwa upya (1-32)</p> <p>4 Kazi yaendelea licha ya upinzani (1-14)
Ujenzi waendelea wajenzi wakiwa na silaha (15-23)</p> <p>5 Nehemia akomesha ukandamizaji (1-13)
Nehemia hakutenda kwa ubinafsi (14-19)</p> <p>6 Kazi ya kujenga upya yaendelea kupingwa (1-14)
Ukuta wakamilika baada ya siku 52 (15-19)</p> <p>7 Malango ya jiji na walinzi wa malango (1-4)
Orodha ya watu waliorudi kutoka uhamishoni (5-69)
Watumishi wa hekaluni (46-56)
Wana wa watumishi wa Sulemani (57-60)</p> | <p>Michango kwa ajili ya kazi (70-73)</p> <p>8 Sheria yasomwa na kufafanuliwa mbele ya watu (1-12)
Sherehe ya Vibanda yaadhimishwa (13-18)</p> <p>9 Watu waungama dhambi zao (1-38)
Yehova, Mungu anayesamehe (17)</p> <p>10 Watu wakubali kuifuata Sheria (1-39)
“Hatutaipuuza nyumba ya Mungu wetu” (39)</p> <p>11 Watu waanza kuishi tena Yerusalemu (1-36)</p> <p>12 Makuhani na Walawi (1-26)
Ukuta wazinduliwa (27-43)
Kutegemeza utumishi wa hekalu (44-47)</p> <p>13 Nehemia afanya marekebisho zaidi (1-31)
Sehemu za kumi zatolewa (10-13)
Sabato isichafuliwe (15-22)
Wakatazwa kuoa watu wa mataifa mingine (23-28)</p> |
|--|---|

1 Maneno ya Nehemia*^a mwana wa Hakalia: Sasa katika mwezi wa Kislevu,[#] mwaka wa 20, mimi nilikuwa katika ngome ya^Δ Shushani.^{Ωb}

2 Wakati huo Hanani,^c mmoja wa ndugu zangu, akaja pamoja

SURA YA 1

a Ne 1:11
Ne 5:14
Ne 10:1b Est 1:2
Est 3:15
Da 8:2

c Ne 7:2

Safu ya 2

a Yer 52:30

na watu wengine kutoka Yuda, nami nikawauliza kuhusu Wayahudi waliobaki walioponyoka kutoka utekwani,^a na pia kuhusu Yerusalemu. **3** Wakanijibu: “Wale waliobaki na kuponyoka utekwani ambao wamebaki katika mkoa* ule,

1:3 *Au “wilaya ya utawala.”

1:1 *Maana yake “Yah Hufariji.” [#]Angalia Nyongeza B15. ^ΔAu “jumba la mfalme la.” ^ΩAu “Susa.”

wako katika hali mbaya sana na yenye kuaibisha.^a Kuta za Yerusalemu zimebomolewa,^b na malango yake yameteketewa kwa moto.”^c

4 Mara tu niliposikia mneni hayo, nikaketi chini na kuanza kulia na kuomboleza kwa siku nyingi, nami nikaendelea kufunga^d na kusali mbele za Mungu wa mbinguni. **5** Nikasema: “Ee Yehova, Mungu wa mbinguni, Mungu mkuu na mwenye kuogopesha, unayeshika agano lako na kuwatendeka kwa upendo mshikamanifu wale wanaokupenda na kushika amri zako,^e **6** tafadhali, tega sikio lako na ufungue macho yako ili usikilize sala ambayo mimi mtumishi wako ninakutolea leo, mchana na usiku,^f kuhusu watumishi wako Waisraeli, nikiungama dhambi ambazo watu wa Israeli wamekutendeka. Tumetenda dhambi, mimi pamoja na nyumba ya baba yangu.^g **7** Kwa hakika tumetenda mambo mapotovu dhidi yako^h kwa kuwa hatukushika amri, masharti, na sheria ulizompa* mtumishi wako Musa.ⁱ

8 “Tafadhali, kumbuka neno ulilomwamuru* Musa mtumishi wako, ukisema: ‘Msipotenda kwa uaminifu, nitawatawanya miongoni mwa mataifa.^j **9** Lakini mkinirudia na kuzishika amri zangu na kuzitii, hata ingawa mtakuwa mmetawanyika mpaka kwenye mwisho wa mbingu, nitawakusanyia^k na kuwaleta mahali ambapo nimepachagua ili jina langu

1:7 *Tnn., “maamuzi ya hukumu uliyo-mwagiza.” 1:8 *Au “onyo ulilompa.”

SURA YA 1

a 1Fa 9:7
Ne 9:36, 37
Zb 79:4

b 2Fa 25:10

c Ne 2:17
Omb 1:4

d 2Nya 20:3
Ezr 8:21

e Kum 7:9
Da 9:4

f Zb 88:1
Lu 18:7

g 2Nya 29:6
Ezr 9:6

h Zb 106:6

i Law 27:34
Hes 36:13
Kum 12:1
Ne 9:34

j Law 26:33
Kum 4:27
Kum 28:64

k Kum 30:1-4

Safu ya 2

a Kum 12:5
Zb 132:13

b Law 25:42
Kum 5:15
Kum 9:26, 29

c 1Fa 8:49, 50
Ezr 7:6
Zb 106:46
Met 21:1

d Ne 2:1

SURA YA 2

e Ne 1:1

f Ezr 7:1
Ne 13:6

g Ne 1:11

h Ne 1:2, 3

i 1Sa 1:13

j Da 9:25

likae hapo.^a **10** Wao ni watumishi wako na watu wako, uliowakomboa kwa uwezo wako mkubwa na kwa mkono wako wenye nguvu.^b **11** Ee Yehova, tafadhali, tega sikio lako usikilize sala yangu mimi mtumishi wako na sala ya watumishi wako wanaofurahia kulihofu jina lako, na tafadhali, nipe mimi mtumishi wako mafanikio leo, ili mtu huyu anihurumie.”^c

Basi mimi nilikuwa msimamizi wa vinywaji vya mfalme.^d

2 Katika mwezi wa Nisani,^e mwaka wa 20^e wa utawala wa Mfalme Artashasta,^f divai ililetwa mbele yake, nami kama kawaida, nikaichukua divai hiyo na kumpa mfalme.^g Lakini sikuwahi kuonekana nikiwa mwenye huzuni mbele yake. **2** Ndipo mfalme akaniambia: “Kwa nini unaonekana umehuzunika sana na wewe si mgonjwa? Lazima una huzuni moyoni.” Ndipo nikao-gopa sana.

3 Kisha nikamwambia mfalme: “Mfalme na aishi muda mrefu! Kwa nini nisiwe na huzuni wakati lile jiji, mahali ambapo mababu zangu wamezikwa ni magofu, na malango yake yameteketewa kwa moto?”^h **4** Ndipo mfalme akaniuliza: “Basi unataka nini?” Mara moja nikasali kwa Mungu wa mbinguni.ⁱ **5** Kisha nikamjibu mfalme: “Ukipenda, Ee mfalme, na ikiwa mimi mtumishi wako nimepata kibali chako, niruhusu niende Yuda, kwenye jiji ambalo mababu zangu wamezikwa ili nilijenge upya.”^j **6** Ndipo mfalme akaniuliza hivi huku

2:1 *Angalia Nyongeza B15.

malkia wake akiwa ameketi kando yake: “Safari yako itachukua muda gani, nawe utarudi lini?” Basi jambo hilo likampendeza mfalme, akaniruhusu niende,^a nami nikamwambia muda hususa.^b

7 Kisha nikamwambia mfalme: “Ukipenda, Ee mfalme, naomba nipewe barua niwapelekee magavana wa eneo lililo Ng’ambo ya Mto,^{*c} ili waniruhusu kupita hadi nifike Yuda salama salimini, **8** pia barua nipelekee Asafu mtunzaji wa Bustani ya Mfalme,^{*} ili anipe mbao za kujengea mihimili ya malango ya Ngo-me^d ya ile Nyumba[#] na kuta za jiji^e na nyumba nitakayoshi.” Basi mfalme akanipa barua hizo,^f kwa sababu mkono mwema wa Mungu wangu ulikuwa juu yangu.^g

9 Mwishowe nikafika kwa magavana wa eneo lililo Ng’ambo ya Mto na kuwapa barua za mfalme. Pia, mfalme alinipa wakuu wa jeshi na wapanda farasi. **10** Sanbalati^h Mhoroni na Tobiaⁱ ofisa* Mwamoni^j waliposikia jambo hilo, walikasirika sana kwa sababu mtu fulani alikuwa amekuja kuwatendea watu wa Israeli jambo jema.

11 Hatimaye nikafika Yerusalemu, nami nikakaa huko kwa siku tatu. **12** Nikaondoka usiku, mimi pamoja na wanaume wachache, nami sikumwambia mtu yeyote mambo ambayo Mungu wangu alikuwa ameweka moyoni mwangu

2:7 *Au “maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati.” 2:8 *Au “msitu wa mfalme.” #Au “Hekalu.” 2:10 *Tnn., “mtumishi.”

SURA YA 2

a Ne 1:11

b Ne 5:14
Ne 13:6c Yos 1:4
Ezr 5:3

d Ne 7:2

e Ne 1:3

f Ezr 7:21

g Ezr 7:6

h Ne 4:1
Ne 6:2i Ne 2:19
Ne 4:3
Ne 6:14
Ne 13:7

j Ne 13:1

Safu ya 2

a 2Nya 26:9

b Ne 3:13

c Ne 1:3
Omb 1:4
Omb 2:9d Ne 3:15
Ne 12:37e 2Sa 15:23
Yoh 18:1

f Ne 4:14

g Ezr 7:6, 28
Ne 2:7, 8

h Da 9:25

ili nilifanyie jiji la Yerusalemu, wala sikuwa na mnyama mwingine ila mnyama aliyenibeba. **13** Nikatoka nje usiku kupitia Lango la Bondeni,^a nikapita mbele ya Chemchemi ya Nyoka Mkubwa, nikaelekea kwenye Lango la Marundo ya Majivu,^b nami nikachunguza kuta za Yerusalemu zilizo kuwa zimebomolewa na malango yake yaliyokuwa yameteketewa kwa moto.^c **14** Kisha nikapita kuelekea kwenye Lango la Chemchemi^d na kuelekea kwenye Kidimbwi cha Mfalme, lakini mnyama aliyenibeba hangeweza kupita kwa sababu hapakuwa na nafasi ya kutosha. **15** Hata hivyo, nikaendelea kupanda juu bondeni^{*e} usiku, nami nikaendelea kuukagua ukuta, nami nikaingia kupitia Lango la Bondeni, kisha nikarudi.

16 Watawala wasaidizi^f hakuwajua nilikokwenda au jambo nililokuwa nikifanya, kwa sababu sikuwa nime-wambia Wayahudi jambo lolote, wala makuhani, wala wakuu, wala watawala wasaidizi, wala wafanyakazi wengineo. **17** Hatimaye nikawaambia: “Mnaona hali mbaya sana tunayokabili, jinsi Yerusalemu lilivyobaki magofu na malango yake yameteketewa kwa moto. Njooi, tujenge upya kuta za Yerusalemu, ili aibu hii isiendelee.” **18** Kisha nikawaambia jinsi mkono mwema wa Mungu wangu ulivyokuwa juu yangu^g na pia maneno ambayo mfalme alikuwa ameniambia.^h Ndipo waka-sema: “Twendeni tukajenge.”

2:15 *Au “korongoni.”

Basi wakaimarishana* ili kufanya kazi hiyo njema.^a

19 Sasa Sanbalati Mhoroni, Tobia^b ofisa* Mwamoni,^c na Geshemu Mwarabu^d waliposikia jambo hilo, wakaanza kutudhiahiki^e na kutudharau wakisema: “Mnafanya nini? Je, mnamwasi mfalme?”^f **20** Lakini nikawajibu: “Mungu wa mbinguni, Ndiye atakayetufanikisha,^g nasi watumishi wake tutasimama na kujenga; lakini ninyi hamna fungu wala haki ya kudai chochote wala kumbukumbu* katika Yerusalemu.”^h

3 Kuhani mkuu Eliashibuⁱ na ndugu zake makuhani wakaanza kujenga Lango la Kondoo.^j Wakalitakasa*^k na kuweka milango yake; wakalitakasa mpaka kwenye Mnara wa Mea,^l na mpaka kwenye Mnara wa Hananeli.^m **2** Sehemu iliyofuata ilikuwa ikijengwa na watu wa Yeriko;ⁿ na sehemu iliyofuata ikajengwa na Zakuri mwana wa Imri.

3 Wana wa Hasenaa wali-jenga Lango la Samaki;^o walilitengeneza kwa mbao,^p wakaweka milango yake, makomeo yake, na mapingo yake.

4 Sehemu iliyofuata ilirekebisha na Meremothi^q mwana wa Uriya mwana wa Hakozi, naye Meshulamu^r mwana wa Berekia mwana wa Mesheza-beli akarekebisha sehemu iliyofuata, naye Sadoki mwana wa Baana akarekebisha sehemu iliyofuata. **5** Sehemu iliyofuata ilirekebisha na Wa-

2:18 *Tnn., “wakaitia nguvu mikono yao.” 2:19 *Tnn., “mtumishi.” 2:20 *Au “haki ya kumiliki.” 3:1 *Au “Wakaliweka wakfu.”

SURA YA 2

a Hag 1:14

b Ne 6:14

c Ne 13:1, 2

d Ne 4:7
Ne 6:1, 2

e Zb 79:4

f Ne 6:6

g Zb 127:1

h Ezz 4:1-3

SURA YA 3

i Ne 12:10
Ne 13:4, 28

j Yoh 5:2

k Ne 12:30

l Ne 12:38, 39

m Yer 31:38
Zek 14:10

n Ezz 2:1, 34

o 2Nya 33:1, 14
Sef 1:10

p Ne 2:7, 8

q Ezz 8:33
Ne 3:21

r Ne 3:30
Ne 6:17, 18

Safu ya 2

a Ne 3:27
Amo 1:1

b Ne 12:38, 39

c 2Sa 21:2

d Yos 18:21, 26
2Nya 16:6
Yer 40:6

e Mwa 15:18

f Ne 12:38

g Ezz 2:1, 32

h Ezz 2:1, 6

i Ne 12:38

tekoa,^a lakini watu wao mashuhuri hawakutaka kujishusha ili kushiriki kufanya* utumishi wa mabwana wao.

6 Yoyada mwana wa Pasea na Meshulamu mwana wa Besodeya wakarekebisha Lango la Jiji la Kale;^b walilitengeneza kwa mbao, wakaweka milango yake, makomeo yake, na mapingo yake. **7** Sehemu iliyofuata ilirekebisha na Melatia Mgibeoni^c na Yadoni Mmeronothi, watu wa Gibeoni na Mispaa,^d waliokuwa chini ya mamlaka ya* gavana wa eneo lililo Ng'ambo ya Mto.^e

8 Sehemu iliyofuata ilirekebisha na Uzieli mwana wa Harhaya, mmoja wa mafundi wa dhahabu, na sehemu iliyofuata ikarekebisha na Hanania, mmoja wa watengenezaji wa marashi,* nao wakatandaza mawe^f Yerusalemu mpaka kwenye Ukuta Mpana.^g **9** Sehemu iliyofuata ilirekebisha na Refaya mwana wa Huru, mkuu wa nusu ya wilaya ya Yerusalemu. **10** Kisha Yedaya mwana wa Harumafu akarekebisha sehemu iliyofuata, yaani, mbele ya nyumba yake mwenyewe, na sehemu iliyofuata ikarekebisha na Hatushi mwana wa Hashabneya.

11 Malkiya mwana wa Harimu^g na Hashubu mwana wa Pahath-moabu^h wakarekebisha sehemu nyingine,* na pia Mnara wa Majiko ya Kuokea.ⁱ **12** Sehemu iliyofuata ilireke-

3:5 *Tnn., “hawakutia shingo zao kwenye.” 3:7 *Tnn., “walio wa kiti cha ufalme cha.” *Au “maeneo yaliyo magharibi ya Mto Efrati.” 3:8 *Au “wachanganyaji wa manukato.” *Au “wakatandaza mabamba ya mawe.” 3:11 *Au “sehemu iliyopimwa.”

bishwa na Shalumu mwana wa Haloheshi, mkuu wa nusu ya wilaya ya Yerusalemu, pamoja na mabinti zake.

13 Hanuni na wakaaji wa Zanoa^a walirekebisha Lango la Bondeni;^b wakalijenga na kuweka milango yake, makomeo yake, na mapingo yake, pia walirekebisha sehemu ya ukuta yenye urefu wa miko-no 1,000* mpaka kwenye Lango la Marundo ya Majivu.^c
14 Malkiya mwana wa Reka-bu, mkuu wa wilaya ya Beth-hakeremu^d alirekebisha Lango la Marundo ya Majivu; akalijenga na kuweka milango yake, makomeo yake, na mapingo yake.

15 Shaluni mwana wa Kolhoze, mkuu wa wilaya ya Mispā,^e alirekebisha Lango la Chemchemi;^f akalijenga na kuweka paa lake, milango yake, makomeo yake, na mapingo yake, na pia alirekebisha ukuta wa Kidimbwi^g cha Mfereji unaoelekea kwenye Bustani ya Mfalme^h mpaka kwenye Ngaziⁱ inayoshuka kutoka Jiji la Daudi.^j

16 Baada yake Nehemia mwana wa Azbuki, mkuu wa nusu ya wilaya ya Beth-suri,^k alirekebisha kuanzia mbele ya Makaburi ya Daudi^l mpaka kwenye kidimbwi^m kilichokuwa kimetengenezwa hadi kwenye Nyumba ya Wenye Nguvu.

17 Walawi walirekebisha sehemu iliyofuata: Rehumu mwana wa Bani; na baada yake Hashabia, mkuu wa nusu ya wilaya ya Keila,ⁿ akarekebisha kwa ajili ya wilaya yake.

3:13 *Mita 445 hivi (futi 1, 460). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 3

a Yos 15:20, 34
Ne 11:25, 30

b 2Nya 26:9

c Ne 2:13

d Yer 6:1

e Yos 18:21, 26

f Ne 2:14
Ne 12:37

g Isa 22:9

h Yer 39:4

i Ne 12:37

j 2Sa 5:7

k Yos 15:20, 58
2Nya 11:5-7

l 1Fa 2:10
2Nya 16:13, 14

m Ne 2:14

n Yos 15:20, 44

Safu ya 2

a 2Nya 26:9
Ne 3:24

b Ezr 2:1, 40

c Ezr 10:28, 44

d Ne 3:1
Ne 13:4

e Ezr 8:33

f Mwa 13:10

g Ne 3:19

h 2Sa 5:11
Ne 12:37

i Yer 37:21

18 Ndugu zao wakarekebisha sehemu iliyofuata: Bavai mwana wa Henadadi, mkuu wa nusu ya wilaya ya Keila.

19 Sehemu iliyofuata, mbele ya njia inayopanda kuelekea Ghala la Silaha karibu na Nguzo ya Kutegemeza Ukuta,^a ilirekebisha na Ezeri mwana wa Yeshua,^b mkuu wa Mispā.

20 Baada yake Baruku mwana wa Zabai^c akafanya kazi kwa bidii na kurekebisha sehemu nyingine, kuanzia Nguzo ya Kutegemeza Ukuta mpaka lango la nyumba ya kuhani mkuu Eliashibu.^d

21 Meremothi^e mwana wa Uriya mwana wa Hakozi alirekebisha sehemu nyingine, kuanzia lango la nyumba ya Eliashibu mpaka mwisho wa nyumba ya Eliashibu.

22 Sehemu iliyofuata ilirekebisha na makuhani, wanaume wa wilaya ya Yordani.^{*f}

23 Kisha Benjamini na Hashubu wakarekebisha mbele ya nyumba yao wenyewe. Na baada yao Azaria mwana wa Maaseya mwana wa Ananiya akarekebisha karibu na nyumba yake. **24** Baada yake Binui mwana wa Henadadi akarekebisha sehemu nyingine, kuanzia nyumba ya Azaria mpaka kwenye Nguzo ya Kutegemeza Ukuta^g na mpaka pembeni.

25 Baada yake Palali mwana wa Uzai akarekebisha mbele ya Nguzo ya Kutegemeza Ukuta na mnara unaotoka katika Nyumba ya Mfalme,^{*h} upande wa juu wa Ua wa Walinzi.ⁱ Baada yake

3:22 *Au labda, "wilaya jirani." 3:25 *Au "Jumba la Mfalme."

kulikuwa na Pedaya mwana wa Paroshi.^a

26 Na watumishi wa hekaluni*^b walioishi Ofeli^c waka-fanya marekebisho hadi mbele ya Lango la Maji^d upande wa mashariki na mnara uliochomoza.

27 Sehemu iliyofuata ilirekebishwa na Watekoa,^e kuto-ka mbele ya ule mnara mkuu uliochomoza mpaka kwenye ukuta wa Ofeli.

28 Makuhani walirekebisha sehemu iliyo juu ya Lango la Farasi,^f kila mmoja mbele ya nyumba yake mwenyewe.

29 Kisha Sadoki^g mwana wa Imeri akarekebisha sehemu iliyokuwa mbele ya nyumba yake.

Na sehemu iliyofuata ikarekebishwa na Shemaya mwana wa Shekania, mlinzi wa Lango la Mashariki.^h

30 Sehemu iliyofuata ilirekebishwa na Hanania mwana wa Shelemia na Hanuni mwana wa sita wa Zalafu.

Naye Meshulamuⁱ mwana wa Berekia akarekebisha sehemu iliyokuwa mbele ya ju-mba lake.

31 Malkiya, mshiriki wa chama cha mafundi wa dhahabu, alirekebisha sehemu iliyofuata mpaka kwenye nyumba ya watumishi wa hekaluni*^j na wafanyabiashara, mbele ya Lango la Ukaguzi mpaka kwenye chumba cha dari cha pembeni.

32 Mafundi wa dhahabu na wafanyabiashara walirekebi-sha sehemu iliyokuwa kati ya chumba cha dari cha pembeni na Lango la Kondoo.^k

3:26, 31 *Au "Wanethini." Tnn., "walio-tolewa."

SURA YA 3

- a Ezr 2:1, 3
- b Yos 9:3, 27
1Nya 9:2
Ezr 2:43-54
Ezr 8:17, 20
- c 2Nya 27:1, 3
2Nya 33:1, 14
Ne 11:21
- d Ne 8:1
Ne 12:37
- e Ne 3:5
- f Yer 31:40
- g Ne 13:13
- h 1Nya 9:17, 18
- i Ne 6:17, 18
- j Ne 3:26
- k Ne 3:1
Yoh 5:2

Safu ya 2

SURA YA 4

- a Ne 2:10
Ne 6:1, 2
Ne 13:28
- b Ne 4:10
- c Ne 2:19
- d Ne 13:1, 2
- e Zb 123:3
- f Zb 79:12
- g Yer 18:23
- h Ne 4:3
- i Ne 2:19
- j Yos 13:2, 3
Ne 13:23

4 Mara tu Sanbalati^a alipo-sikia kwamba tunajenga upya ukuta, alishikwa na gha-dhabu na kukasirika sana,* naye akazidi kuwadhihaki Wayahudi. **2** Akasema hivi mbele ya ndugu zake na jeshi la Samaria: "Wayahudi hawa wanyonge wanafanya nini? Je, watafanya kazi hii peke yao? Je, watatoa dhahabu? Je, watamaliza kwa siku moja? Je, watayatoa mawe yaliyoungua kutoka katika marundo ya vifusi ili yafae kwa ujenzi?"^b

3 Basi Tobia^c Mwamoni,^d aliyekuwa amesimama kando yake, akasema: "Hata mbweha akipanda juu ya kile wana-chojenga, atauangusha ukuta wao wa mawe."

4 Sikiliza, Ee Mungu wetu, kwa maana tunadharauliwa;^e na urudishe dharau yao juu ya vichwa vyao wenyewe,^f nawe uwafanye wawe nyara na mateka katika nchi nyingine. **5** Usiifunike hatia yao wala usiifute dhambi yao kutoka mbele zako,^g kwa maana wamewatukana wajenzi.

6 Basi tukaendelea kuje-nga, na ukuta wote ukaunga-na kufikia nusu ya kimo cha-ke, nao watu wakaendelea ku-fanya kazi kwa moyo wote.

7 Sasa mara tu Sanbalati, Tobia,^h Waarabu,ⁱ Waamoni, na Waashdodi^j waliposikia kwamba kazi ya kurekebisha kuta za Yerusalemu inasonga mbele na kwamba mianya ilikuwa ikizibwa, wakakasirika sana. **8** Wakapanga njama pamoja ili kupigana na Yerusalemu na kuleta vurugu humo. **9** Lakini tulisali

4:1 *Au "aliudhika."

kwa Mungu wetu na kuweka walinzi dhidi yao mchana na usiku.

10 Hata hivyo, watu wa Yuda walikuwa wakisema: “Wafanyakazi* wameishiwa na nguvu, na kuna vifusi vingi sana; hatutafaulu kamwe kuu-jenga ukuta.”

11 Maadui wetu wakaendelea kusema: “Kabla hawajajua au kutuona, tutaingia kati yao, tuwae, na kuikomesha kazi.”

12 Kila mara Wayahudi walioishi karibu nao walipokuja, walikuwa wakituambia tena na tena:* “Watatushambulia kutoka kila upande.”

13 Basi nikaweka wanaume kwenye sehemu za chini zaidi zilizo wazi nyuma ya ukuta, nikawapanga kulingana na familia zao, wakiwa na mapanga yao, mikuki yao, na pinde zao. **14** Nilipoona jinsi walivyoogopa, mara moja nikasimama na kuwaambia wakuu^a na watawala wasaidizi na watu wengine wote: “Msiwaogope.^b Mkumbukeni Yehova, ambaye ni mkuu na mwenye kuogopesha;^c nanyi mpi-gane kwa ajili ya ndugu zenu, wana wenu na mabinti zenu, wake zenu na nyumba zenu.”

15 Sasa baada ya maadui wetu kusikia kwamba tunajua walichokuwa wakifanya na kwamba Mungu wa kweli alikuwa amevuruga mpango wao, sote tukarudi kuujenga ukuta. **16** Tangu siku hiyo na kuendelea, nusu ya wanau-me wangu walikuwa wakifanya kazi^d na nusu nyingine walikuwa wakishika mikuki,

4:10 *Au “Wabeba mizigo.” 4:12 *Tnn., “mara kumi.”

SURA YA 4

a Ne 13:17

b Hes 14:9
Kum 20:3
Yos 1:9

c Kum 7:21
Kum 10:17

d Ne 5:16

Safu ya 2

a Ne 11:1

b Hes 10:9
2Nya 13:12

c Kum 1:30
Yos 23:10

d Ne 13:19

SURA YA 5

e Kum 15:9

ngao, pinde, na kuvaa makoti ya vita. Na wakuu^a walisi-mama nyuma ya watu wote wa nyumba ya Yuda **17** walioku-wa wakijenga ukuta. Watu waliokuwa wakibeba mizigo walifanya kazi kwa mkono mmoja, huku wakiwa wameshika silaha kwa mkono mwingine. **18** Na kila mjenzi alikuwa amejifunga upanga kiunoni huku akijenga, na mtu wa kupiga pembe^b alikuwa amesimama kando yangu.

19 Ndipo nikawaambia wakuu na watawala wasaidizi na watu wengine wote: “Kazi hii ni kubwa na nzito, nasi tumetawanyika kwenye ukuta kila mmoja mbali na mwenzake. **20** Mtakaposikia mlio wa pembe, kusanyikeni mahali tulipo. Mungu wetu atatupigania.”^c

21 Basi tukaendelea kufanya kazi huku nusu ya wanau-me wakiwa wameshika mikuki, kuanzia mapambazuko mpaka nyota zilipoonekana. **22** Wakati huo nikawaambia watu: “Kila mwanamume na mtumishi wake na wakae ndani ya Yerusalemu usiku, nao watakuwa walinzi usiku na watafanya kazi mchana.” **23** Basi mimi, ndugu zangu, watumishi wangu,^d na walinzi waliofuatana nami hatukuvua mavazi yetu kamwe, na kila mmoja wetu aliendelea kushika silaha yake kwa mkono wa kulia.

5 Hata hivyo, watu na wake zao wakaanza kulalamika sana kuhusu ndugu zao Wayahudi.^e **2** Baadhi yao walikuwa wakisema: “Sisi na wana wetu na mabinti zetu ni wengi. Tunahitaji nafaka ili tule

tuendelee kuishi.” **3** Na wengine walikuwa wakisema: “Tunatoa mashamba yetu na mashamba yetu ya mizabibu na nyumba zetu kuwa rehani ili tupate nafaka wakati wa njaa.” **4** Na wengine walikuwa wakisema: “Tumekopa pesa kwa kuweka rehani mashamba yetu na mashamba yetu ya mizabibu ili kulipa ushuru wa mfalme.” **5** Sasa sisi na ndugu zetu ni watu wa mwili mmoja na damu moja,* na watoto wetu ni sawa na watoto wao; lakini tumelazimika kuwafanya wana na mabinti zetu kuwa watumwa, na baadhi ya mabinti zetu tayari wako utumwani.^b Na hatuna uwezo wa kuzuia jambo hili, kwa sababu mashamba yetu na mashamba yetu ya mizabibu yamechukuliwa na wengine.”

6 Nilikasirika sana niliposikia kilio chao na maneno hayo. **7** Kwa hiyo nikatafakiri mambo hayo moyoni mwangu, kisha nikawashutumu wakuu na watawala wasaidizi na kuwaambia: “Kila mmoja wenu anamtoza riba* ndugu yake mwenyewe.”^c

Pia, nikapanga kusanyiko kubwa kwa sababu yao. **8** Nikawaambia: “Kwa kadiri tulivyoweza, tumewanua ndugu zetu wenyewe, Wayahudi, waliouzwa kwa mataifa; lakini je, sasa mtawauza ndugu zenu wenyewe,^d nasi tulazimike kuwanunua tena?” Ndipo wakanyamaza kimya, hawakuwa na lolote la ku-

5:5 *Tnn., “nyama ya mwili wa ndugu zetu ni sawa na nyama ya mwili wetu.”
5:7 *Au “faida.”

SURA YA 5

a Kum 28:15, 33
Ne 9:36, 37

b Kut 21:7
Kum 15:12

c Kut 22:25
Kum 23:19
Zb 15:5
Eze 22:12

d Law 25:35
Kum 15:7, 8
Yer 34:8, 9

Safu ya 2

a Law 25:36
Ne 5:15

b Eze 18:5, 8

c Ne 5:3

d Ne 10:1

e Ne 2:1

f Ne 13:6

g Eze 8:1

h 1Ko 9:14, 15
2Th 3:8

9 Kisha nikawaambia: “Jambo mnalofanya si jema. Je, hampaswi kutembea kwa kumwogopa Mungu^a wetu ili mataifa, maadui wetu, wasitushutumu? **10** Zaidi ya hayo, mimi, ndugu zangu, na watumishi wangu tunawakopesha pesa na nafaka. Tafadhali, tuache kukopesha kwa riba.”^b **11** Tafadhali, warudishieni leo hii mashamba yao,^c mashamba yao ya mizabibu, na mizeituni yao, na nyumba zao, na pia sehemu moja ya mia* ya pesa zao, nafaka, divai mpya, na mafuta mnayowadai kama riba.”

12 Ndipo wakasema: “Tutarudishia vitu hivyo bila kuwadai chochote. Tutafanya sawasawa na ulivyotuagiza.” Basi nikawaita makuhani na kuwaapisha wanaume hao ili watimize ahadi hiyo. **13** Pia, nikakung’uta vazi langu* na kusema: “Mungu wa kweli na amkung’ute hivi kutoka nyumbani mwake na kutoka katika mali zake kila mwanamume ambaye hatatimiza ahadi hii, na akung’utwe hivi na kubaki bila chochote.” Ndipo kutaniko lote likajibu: “Amina!”[#] Wakamsifu Yehova, na watu wakafanya kama walivyoahidi.

14 Isitoshe, tangu siku mfalme aliponiteua kuwa gavana^d katika nchi ya Yuda, kuanzia mwaka wa 20^e mpaka mwaka wa 32^f wa utawala wa Mfalme Artashasta,^g miaka 12, mimi na ndugu zangu hatukula chakula kilichokuwa haki ya gavana.^h **15** Lakini

5:11 *Au “asilimia moja,” yaani, kila mwezi. 5:13 *Tnn., “nikatikisa kifua changu.” *Au “Na iwe hivyo!”

magavana walionitangulia waliwalemea watu, kila siku walichukua kutoka kwao shekeli 40 za fedha* kwa ajili ya mkate na divai. Pia, watumishi wao waliwakandamiza watu. Lakini mimi sikufanya hivyo^a kwa sababu nilimwogopa Mungu.^b

16 Isitoshe, mimi pia nilishiriki kujenga ukuta huu, nasi hatukuchukua hata shamba moja;^c watumishi wangu wote walikusanyika hapo ili kufanya kazi. **17** Kulikuwa na Wayahudi na watawala wasaidizi 150 waliokula kwenye meza yangu, na pia watu waliokuja kwetu kutoka mataifa jirani. **18** Kila siku nilitayarishiwa* ng'ombe dume mmoja, kondoo sita walio bora, na ndege wengi, na kila baada ya siku kumi tuliandaliwa kwa wingi divai ya kila aina. Licha ya hayo sikudai chakula kilichokuwa haki ya gavana, kwa kuwa tayari watu walikuwa wamelemewa na kazi. **19** Ee Mungu wangu, nikumbuke na kunitendea wema,* kwa ajili ya yote niliyowatendea watu hawa.^d

6 Sasa mara tu Sanbalati, Tobia,^e Geshemu Mwarabu,^f na maadui wetu wengine wote walipoambiwa kwamba nimejenga upya^g ukuta na hakuna mwanya wowote ukutani (ingawa kufikia wakati huo sikukuwa nimeweka milango kwenye malango),^h **2** mara moja Sanbalati na Geshemu wakanitumia ujumbe wakisema:

5:15 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. 5:18 *Au "Kila siku nilitayarishiwa kwa gharama yangu." 5:19 *Au "na kunipa kibali."

SURA YA 5

a 2Ko 11:9
2Ko 12:14

b Ne 5:9

c Mdo 20:33
2Ko 12:17

d Ne 13:14
Zb 18:24
Isa 38:3
Mal 3:16

SURA YA 6

e Ne 2:10
Ne 4:3

f Ne 2:19
Ne 4:7

g Da 9:25

h Ne 3:1, 3

Safu ya 2

a 1Nya 8:12
Ne 11:31, 35

b Ne 2:19

c Ezz 4:14, 15

d Ezz 4:4

e Zb 68:35
Zb 138:3
Isa 41:10

"Njoo, tupange wakati ili tukutane kwenye vijiji vya Bonde Tambarare la Ono."^a Lakini walikuwa wakipanga njama ya kunidhuru. **3** Basi nika-watuma wajumbe kwao niki-sema: "Ninafanya kazi kubwa sana, siwezi kushuka chini. Kwa nini kazi isimame ili nije kwenu?" **4** Wakanitumia ujumbe uleule mara nne, nami nikawapa jibu lilelile kila mara.

5 Kisha Sanbalati akamtuma mtumishi wake kwangu akiwa na ujumbe uleule mara ya tano, akaja na barua iliyo-kuwa wazi mkononi mwake. **6** Ilikuwa imeandikwa hivi: "Kuna habari zinazoenezwa katika mataifa, na Geshemu^b anasema pia kwamba wewe na Wayahudi mnapanga kuasi.^c Hii ndiyo sababu unajenga ukuta; na kulingana na habari hizo unataka kuwa mfalme wao. **7** Pia, umeweka manabii ili watangaze kukuhusu kotekote Yerusalemu, 'Kuna mfalme katika Yuda!' Na sasa mfalme atajulishwa mambo haya. Basi njoo, tuzungumzie jambo hili pamoja."

8 Hata hivyo, nikamtumia jibu hili: "Hakuna jambo lolote unalosema ambalo limetendeka; umeyabuni wewe mwenyewe."^{**} **9** Kwa maana wote walikuwa wakijaribu kutuogopesha, wakisema: "Mikono yao italegea kazini, na kazi hiyo haitafanywa."^d Sasa, ninasali, itie nguvu mikono yangu.^e

10 Kisha nikaenda nyumbani kwa Shemaya mwana wa Delaya mwana wa Mehetabeli, alipokuwa amejifungia ndani. Akasema: "Tupange wakati ili

6:8 *Tnn., "yanatoka moyoni mwako."

tukutane katika nyumba ya Mungu wa kweli, ndani ya hekalu, nasi tufunge milango ya hekalu, kwa maana wanakuja kukuua. Wanakuja kukuua usiku.” **11** Lakini nikasema: “Je, mtu kama mimi anapaswa kukimbia? Je, mtu kama mimi anaweza kuingia hekalu ni na aendelee kuishi?^a Sitainingia!” **12** Ndipo nikatambua kwamba Mungu hakuwa amemtuma, bali Tobia na Sanbalati^b walikuwa wamemkodi ili atabiri maneno hayo kunihusu. **13** Alikuwa amekodiwa ili aniogopeshe na kunifanya nitende dhambi, kisha wawe na sababu ya kuniharibia sifa ili wanishutumu.

14 Ee Mungu wangu, mku mbuke Tobia^c na Sanbalati na matendo haya yote, na pia Noadia yule nabii wa kike na manabii wengine ambao daima walijaribu kuniogopesha.

15 Mwishowe ukuta ulikamilishwa katika siku ya 25 ya mwezi wa Eluli,* kwa muda wa siku 52.

16 Mara tu maadui wetu wote waliposikia habari hiyo na mataifa yote jirani yalipoona jambo hilo, wakaabika sana,^d nao wakatambua kwamba kazi hii ilikuwa imefanjwa kwa msaada wa Mungu wetu. **17** Siku hizo wakuu^e wa Yuda walikuwa wakimtumia Tobia barua nyingi, naye alikuwa akiwajibu. **18** Watu wengi huko Yuda walikuwa wameapa kumuunga mkono, kwa sababu alikuwa amemwoa binti ya Shekania mwana wa Ara,^f na Yehohani mwanawe alikuwa ame-

6:15 *Angalia Nyongeza B15.

SURA YA 6

a Hes 1:51
Hes 18:7
2Nya 26:18, 19

b Ne 2:10

c Ne 4:3, 4

d Ne 4:7
Zb 129:5

e Ne 5:7

f Ezz 2:1, 5

Safu ya 2

a Ne 3:4

b Ne 6:9
Ne 6:10, 13

SURA YA 7

c Ne 2:17
Ne 6:15
Da 9:25

d Ne 3:1, 6, 13

e 1Nya 26:1
Ezz 2:1, 42

f 1Nya 9:33
Ezz 2:1, 41

g Ezz 3:8

h Ne 1:2

i Ne 2:8

j Ne 5:15

k Ne 11:1

l 1Nya 9:1
Ezz 2:59, 62

mwoa binti ya Meshulam^a mwana wa Berekia. **19** Pia, kila mara walikuwa wakiniambia mambo mema kumhusu na kumjulisha mambo niliyosema. Naye Tobia alikuwa akinitumia barua za kuniogopesha.^b

7 Mara tu ukuta ulipojengwa upya^c nikaweka milango;^d kisha walinzi wa malango,^e waimbaji,^f na Walawi^g wakawekwa rasmi. **2** Kisha nikamweka ndugu yangu Hanani^h asimamie Yerusalemu, pamoja na Hanania mkuu wa Ngome,ⁱ kwa maana alikuwa mwanamume mwaminifu zaidi na alimwogopa Mungu wa kweli^j kuliko watu wengine wengi. **3** Basi nikawaambia: “Malango ya Yerusalemu yasi-funguliwe mpaka mchana kabisa, na wanapolinda wanapaswa kufunga milango na kuweka makomeo. Kisha wapange wakaaji wa Yerusalemu wawe walinzi, kila mmoja katika kituo chake cha ulinzi alichogawiwa na kila mmoja mbele ya nyumba yake.” **4** Sasa jiji lilikuwa kubwa na pana, na watu walikuwa wachache,^k na nyumba hazikuwa zimejengwa upya.

5 Lakini Mungu wangu akaweka wazo moyoni mwangu niwakusanye wakuu, watawala wasaidizi, na watu ili waandikishwe kulingana na ukoo wao.^l Kisha nikapata kitabu cha orodha za koo za wale waliokuja mwanzoni, na kilikuwa na habari zifuatazo:

6 Hawa ndio watu wa mkoa* waliopanda kutoka utekwani huko uhamishoni,

7:6 *Au “wilaya ya utawala.”

ambao Mfalme Nebukadnezar^a wa Babiloni alikuwa amewa-peleka uhamishoni^b na ambao baadaye walirudi Yerusalemu na Yuda, kila mmoja kwenye jiji lake,^c **7** wale waliokuja na Zerubabeli,^d Yeshua,^e Nehemia, Azaria, Raamia, Nahamani, Mordekai, Bilshani, Misperethi, Bigvai, Nehumu, na Baana.

Idadi ya wanaume Waisraeli ilitia ndani:^f **8** wana wa Paroshi, 2,172; **9** wana wa Shefatia, 372; **10** wana wa Ara,^g 652; **11** wana wa Pahathmoabu,^h wa wana wa Yeshua na Yoabu,ⁱ 2,818; **12** wana wa Elamu,^j 1,254; **13** wana wa Zatu, 845; **14** wana wa Zakai, 760; **15** wana wa Binui, 648; **16** wana wa Bebai, 628; **17** wana wa Azgadi, 2,322; **18** wana wa Adonikamu, 667; **19** wana wa Bigvai, 2,067; **20** wana wa Adini, 655; **21** wana wa Ateri, wa Hezekia, 98; **22** wana wa Hashumu, 328; **23** wana wa Besai, 324; **24** wana wa Harifu, 112; **25** wana wa Gibeoni,^k 95; **26** wanaume wa Bethlehemu na Netofa, 188; **27** wanaume wa Anathothi,^l 128; **28** wanaume wa Bethazmavethi, 42; **29** wanaume wa Kiriath-yearimu,^m Kefira, na Beerothi,ⁿ 743; **30** wanaume wa Rama na Geba,^o 621; **31** wanaume wa Mikmasi,^p 122; **32** wanaume wa Betheli^q na Ai,^r 123; **33** wanaume wa ile Nebo nyingine, 52; **34** wana wa Elamu mwingine, 1,254; **35** wana wa Harimu, 320; **36** wana wa Yeriko, 345; **37** wana wa Lodi, Haddi, na Ono,^s 721; **38** wana wa Senaa, 3,930.

SURA YA 7

a 2Fa 25:1
Da 3:1

b 2Fa 24:12, 14
2Nya 36:17, 20
Yer 39:9
Yer 52:15, 28

c Ezr 2:1

d Ezr 1:8, 11
Zek 4:9
Mt 1:12

e Ezr 3:8
Ezr 5:2
Hag 1:14
Zek 3:1

f Ezr 2:2-35

g Ne 6:17, 18

h Ezr 10:30, 44

i Ezr 8:1, 9

j Ezr 10:26, 44

k Yos 11:19
2Sa 21:2
Ne 3:7

l Yos 21:8, 18
Yer 1:1

m 1Sa 7:2

n Yos 18:25, 28

o Yos 18:21, 24

p 1Sa 13:5

q 1Fa 12:32

r Yos 7:2

s Ne 6:2
Ne 11:31, 35

Safu ya 2

a Ezr 2:36-39

b Ezr 10:22, 44

c 1Nya 24:3, 8

d Ezr 2:40

e Ezr 3:9

f 1Nya 25:7
Ezr 2:41

g 1Nya 6:31, 39

h Ezr 2:42
Ne 7:1

i 1Nya 9:2, 17
Ne 11:19
Ne 12:25

j Yos 9:3, 27
1Nya 9:2
Ezr 2:43-54
Ezr 2:58

k Ezr 2:55-58
Ne 11:3

39 Makuhani:^a wana wa Yedaya wa nyumba ya Yeshua, 973; **40** wana wa Imeri, 1,052; **41** wana wa Pashuri,^b 1,247; **42** wana wa Harimu,^c 1,017.

43 Walawi:^d Wana wa Yeshua, wa nyumba ya Kadmieli,^e wa wana wa Hodeva, 74; **44** Waimbaji:^f wana wa Asafu,^g 148. **45** Walinzi wa malango:^h wana wa Shalumu, wana wa Ateri, wana wa Talmoni, wana wa Akubu,ⁱ wana wa Hatita, wana wa Shobai, 138.

46 Watumishi wa hekaluni:^{*j} Wana wa Siha, wana wa Hasufa, wana wa Tabaothi, **47** wana wa Kerosi, wana wa Sia, wana wa Padoni, **48** wana wa Lebana, wana wa Hagaba, wana wa Salmi, **49** wana wa Hanani, wana wa Gideli, wana wa Gahari, **50** wana wa Reaya, wana wa Resini, wana wa Nekoda, **51** wana wa Gazamu, wana wa Uza, wana wa Pasea, **52** wana wa Besai, wana wa Meunimu, wana wa Nefushesimu, **53** wana wa Bakbuki, wana wa Hakufa, wana wa Harhuri, **54** wana wa Baslithi, wana wa Mehida, wana wa Harsha, **55** wana wa Bar-kosi, wana wa Sisera, wana wa Tema, **56** wana wa Nezia, wana wa Hatifa.

57 Wana wa watumishi wa Sulemani:^k wana wa Sotai, wana wa Soferethi, wana wa Perida, **58** wana wa Yaala, wana wa Darkoni, wana wa Gideli, **59** wana wa Shefatia, wana wa Hatili, wana wa Pokereth-hazebaimu, wana wa

7:46 *Au "Wanethini." Tnn., "Waliotolewa."

Amoni. **60** Watumishi wote wa hekaluni*^a na wana wa watumishi wa Sulemani walikuwa 392.

61 Na hawa ndio waliopanda kutoka Tel-mela, Tel-harsha, Kerubi, Adoni, na Imeri, lakini hawakuweza kuthibitisha kama ukoo wao* na asili yao ilikuwa ya Waisraeli;^b

62 wana wa Delaya, wana wa Tobia, wana wa Nekoda, **642.**

63 Na kutoka kwa makuhani: wana wa Habaya, wana wa Hakozu,^c wana wa Barzilai,^d aliye-mwoa mmoja kati ya mabinti wa Barzilai Mgileadi na kuitwa kwa jina lao. **64** Hao walichunguza kumbukumbu zao ili wathibitisha ukoo wao, lakini hawakupata majina ya koo zao, kwa hiyo hawakustahili kuwa makuhani.*^e **65** Gavana^f akawaambia kwamba hapapaswi kula vitu vitakatifu kabisa^g mpaka apatikane kuhani ambaye angechunguza Urimu na Thumimu.^h

66 Kutaniko lote lilikuwa na jumla ya watu 42,360,ⁱ **67** mbali na watumwa wao wa kiume na wa kike,^j ambao walikuwa 7,337; walikuwa pia na waimbaji 245 wa kiume na wa kike.^k **68** Walikuwa na farasi 736, nyumbu 245, **69** ngamia 435, na punda 6,720.

70 Baadhi ya viongozi wa koo* walitoa mchango kwa ajili ya kazi.^l Gavana[#] alitoa kwa ajili ya hazina drak-

ma 1,000 za dhahabu,* mabakuli 50, na kanzu 530 za makuhani.^a **71** Na baadhi ya viongozi wa koo* walitoa kwa ajili ya hazina ya kazi drakma 20,000 za dhahabu na mina 2,200 za fedha.[#] **72** Na wale watu wengine walitoa drakma 20,000 za dhahabu, mina 2,000 za fedha, na kanzu 67 za makuhani.

73 Na makuhani, Walawi, walinzi wa malango, waimbaji,^b baadhi ya watu, watumishi wa hekaluni,* na Waisraeli wengine wote wakaanza kuisi katika majiji yao.^c Kufikia mwezi wa saba,^d Waisraeli wote[#] walikuwa wakiishi katika majiji yao.^e

8 Kisha watu wote wakakusanyika wakiwa na kusudi moja katika uwanja wa jiji uliokuwa mbele ya Lango la Maji,^f wakamwambia Ezra^g mwandishi* alete kitabu cha Sheria ya Musa,^h ambayo Yehova alikuwa ameamuru Waisraeli waifuata.ⁱ **2** Basi kuhani Ezra akaleta Sheria mbele ya kutaniko^j la wanaume, wanawake, na wote walioweza kusikiliza na kuelewa, katika siku ya kwanza ya mwezi wa saba.^k **3** Naye akaisoma kwa sauti kubwa^l katika uwanja wa jiji mbele ya Lango la Maji, kuanzia asubuhi hadi aduhuri, akawasomea wanaume, wanawake, na

7:60 *Au "Wanethini wote." Tnn., "Wote Waliotolewa." **7:61, 70, 71** *Yaani, ukoo wa upande wa baba. **7:64** *Au "hawakustahili utumishi wa kikuhanu kwa sababu hawakuwa safi." **7:65, 70** #Au "Tirshatha," cheo cha Kiajemi cha gavana wa mkoa.

SURA YA 7

a Yos 9:3, 27
Ne 3:26

b Ezz 2:59-63

c 1Nya 24:3, 10
Ne 3:21

d 2Sa 17:27-29
2Sa 19:31
1Fa 2:7

e Hes 18:7

f Ne 8:9
Ne 10:1

g Law 2:3
Hes 18:8, 9

h Kut 28:30
1Sa 28:6

i Ezz 2:64-67

j Law 25:44

k Kut 15:21
1Sa 18:6

l Ezz 2:68, 69

Safu ya 2

a Law 6:10

b Ne 7:1

c Ne 11:20

d Law 23:24, 27
1Fa 8:2
Ezz 3:1

e Ezz 2:70

SURA YA 8

f Ne 3:26
Ne 12:37

g Ezz 7:6

h Kum 31:9
Yos 1:8

i Law 27:34

j Kum 31:12
2Nya 17:8, 9
Mal 2:7

k Law 23:24
1Fa 8:2

l Mdo 13:15
Mdo 15:21

ma 1,000 za dhahabu,* mabakuli 50, na kanzu 530 za makuhani.^a **71** Na baadhi ya viongozi wa koo* walitoa kwa ajili ya hazina ya kazi drakma 20,000 za dhahabu na mina 2,200 za fedha.[#] **72** Na wale watu wengine walitoa drakma 20,000 za dhahabu, mina 2,000 za fedha, na kanzu 67 za makuhani.

73 Na makuhani, Walawi, walinzi wa malango, waimbaji,^b baadhi ya watu, watumishi wa hekaluni,* na Waisraeli wengine wote wakaanza kuisi katika majiji yao.^c Kufikia mwezi wa saba,^d Waisraeli wote[#] walikuwa wakiishi katika majiji yao.^e

8 Kisha watu wote wakakusanyika wakiwa na kusudi moja katika uwanja wa jiji uliokuwa mbele ya Lango la Maji,^f wakamwambia Ezra^g mwandishi* alete kitabu cha Sheria ya Musa,^h ambayo Yehova alikuwa ameamuru Waisraeli waifuata.ⁱ **2** Basi kuhani Ezra akaleta Sheria mbele ya kutaniko^j la wanaume, wanawake, na wote walioweza kusikiliza na kuelewa, katika siku ya kwanza ya mwezi wa saba.^k **3** Naye akaisoma kwa sauti kubwa^l katika uwanja wa jiji mbele ya Lango la Maji, kuanzia asubuhi hadi aduhuri, akawasomea wanaume, wanawake, na

7:70 *Kwa kawaida ilikuwa sawa na dariki ya dhahabu ya Uajemi yenye uzito wa gramu 8.4. Si drakma inayotajwa katika Maandiko ya Kigiriki. Angalia Nyongeza B14. **7:71** #Mina inayotajwa katika Maandiko ya Kiebrania ilikuwa na uzito wa gramu 570. Angalia Nyongeza B14. **7:73** *Au "Wanethini." Tnn., "waliotolewa." #Tnn., "Israeli yote." **8:1** *Au "aliyenakili maandishi."

wote ambao wangeweza kuelewa; nao watu wakasikiliza kwa makini^a kitabu cha Sheria. **4** Na Ezra mwandishi* alikuwa amesimama juu ya juukwaa la mbao, lililotengenezwa kwa kusudi hilo; na Matithia, Shema, Anaya, Uria, Hilikia, na Maaseya walisimama upande wake wa kulia; na upande wake wa kushoto Pedaya, Mishaeli, Malkiya,^b Hashumu, Hash-badana, Zekaria, na Meshulamu.

5 Ezra akakifungua kitabu mbele ya watu wote, kwa maana alikuwa juu kuliko watu wote. Alipokuwa akikifungua, watu wote wakasimama. **6** Kisha Ezra akamsifu Yehova Mungu wa kweli, Aliye mkuu, kisha watu wote wakajibu, "Amina!* Amina!"^c nao wakainua mikono yao juu. Kisha wakamsujudia Yehova huku nyuso zao zikigusa ardhi. **7** Nao Yeshua, Bani, Sherebia,^d Yamini, Akubu, Shabethai, Hodia, Maaseya, Kelita, Azaria, Yozabadi,^e Hanani, na Pelaya, waliokuwa Walawi, walikuwa wakiwafanulia watu Sheria,^f huku watu wakiwa wamesimama. **8** Wakaendelea kukisoma kitabu hicho kwa sauti kubwa, wakaisoma Sheria ya Mungu wa kweli, huku wakiifanua waziwazi na kueleza maana yake; hivyo wakawasaidia watu kuelewa mambo yaliyokuwa yakisomwa.^g

9 Na Nehemia ambaye alikuwa gavana,^h Ezra^h aliye-

8:4, 9, 13 *Au "aliyenakili maandishi." **8:6** *Au "Na iwe hivyo!" **8:8** *Au "wakaeleza maana ya usomaji huo." **8:9** ^hAu "Tirshatha," cheo cha Kiajemi cha gavana wa mkoa.

SURA YA 8

a Mdo 16:14
Mdo 17:11

b Ne 12:40, 42

c Kum 27:26

d Ne 9:4

e Ezz 8:33
Ne 11:16

f Kum 33:8, 10

g Lu 24:27
Mdo 8:30, 31

h Ezz 7:11

Safu ya 2

a Law 23:24

b Est 9:19

c Zb 126:1-3

d Ne 8:8

e Law 23:34, 42
Kum 16:13, 16
Yoh 7:2

f Law 23:4

kuwa kuhani na mwandishi,* na Walawi waliokuwa wakiwafundisha watu wakawaambia hivi watu wote: "Hii ni siku takatifu kwa Yehova Mungu wenu.^a Msiomboleze wala kulia." Kwa maana watu wote walikuwa wakilia walipokuwa wakisikiliza maneno ya Sheria. **10** Akawaambia: "Nendeni mkale vitu bora* na kunywa vitu vitamu, na muwapelekee mafungu ya vyakula^b wale ambao hawana chochote; kwa maana hii ni siku takatifu kwa Bwana wetu, nanyi msihuzunike, kwa maana shangwe ya Yehova ndiyo ngome^c yenu." **11** Nao Walawi walikuwa wakiwatuliza watu wote, wakisema: "Nyamazen! kwa maana hii ni siku takatifu, nanyi msihuzunike." **12** Basi watu wote wakaenda zao kula na kunywa na kupeana mafungu ya chakula na kushangilia sana,^c kwa maana walielewa maneno waliyokuwa wameambiwa.^d

13 Siku iliyofuata viongozi wa koo^e za watu wote, makuhani, na Walawi wakakusanyika karibu na Ezra mwandishi* ili wapate ufahamu zaidi wa maneno ya Sheria. **14** Kisha wakaona imeandikwa katika Sheria kwamba Yehova alikuwa ameamuru kupitia Musa kwamba Waisraeli wanapaswa kukaa katika vibanda* wakati wa sherehe, mwezi wa saba,^e **15** na kwamba wanapaswa kutangaza^f katika majiji yao yote na kotekote Yerusalem wakisema: "Nendeni katika eneo lenye milima

8:10 *Tnn., "vitu vinono." ^eAu "nguvu." **8:13** ^eYaani, ukoo wa upande wa baba. **8:14** *Au "vibanda vya muda."

mlete matawi ya mizeituni, ya misonobari, ya mihadasi na ya mitende, na matawi ya miti mingine yenye majani mengi ili mjenge vibanda, kama ili-vyoandikwa.”

16 Basi watu wakaenda kuleta matawi hayo ili kujijengea vibanda, kila mtu juu ya paa lake, na pia katika nyua zao, na katika nyua za nyumba ya Mungu wa kweli,^a na katika uwanja wa jiji wa Lango la Maji,^b na katika uwanja wa jiji wa Lango la Efraimu.^c

17 Basi watu wote wa kutaniko waliokuwa wamerudi kutoa utekwani wakajenga vibanda nao wakakaa katika vibanda hivyo, kwa maana Waisraeli hawakuwa wamefanya hivyo tangu siku ya Yohua^d mwana wa Nuni mpaka siku hiyo, basi wakashangilia sana.^e **18** Na siku baada ya siku kitabu cha Sheria ya Mungu wa kweli kilikuwa kikisomwa,^f tangu siku ya kwanza hadi siku ya mwisho. Nao wakafanya sherehe hiyo kwa siku saba, na siku ya nane walifanya kusanyiko takatifu, kama ilivyoagizwa.^g

9 Siku ya 24 ya mwezi huo, Waisraeli wakakusanyika; walikuwa wamefunga wakiwa wamevaa nguo za magunia na kujirushia mavumbi.^h **2** Kisha wazao wa Waisraeli waka-jitenga na wageni wote,ⁱ wakasimama na kuungama dhambi zao wenyewe na makosa ya baba zao.^j **3** Kisha wakasimama mahali walipokuwa na kusoma kwa sauti kitabu cha Sheria^k ya Yehova Mungu wao kwa robo siku;^{*} na kwa robo

9:3 *Au “kwa saa tatu.”

SURA YA 8

a 1Fa 6:36
1Fa 7:12
2Nya 4:9
2Nya 20:5

b Ne 3:26
Ne 8:1, 3

c 2Fa 14:13
Ne 12:38, 39

d Yos 1:1

e Kum 16:14, 15

f Kum 31:10-12

g Law 23:34, 36

SURA YA 9

h Yos 7:6
Yon 3:5, 6

i Ezz 9:1, 2
Ne 13:3

j Law 26:40
Ezz 9:6
Zb 106:6
Da 9:8

k Ne 8:3, 8

Safu ya 2

a Ne 8:7

b Ne 8:4

c Yer 33:10, 11

d Kum 6:4

e Mwa 12:1, 2

f Mwa 11:31

g Mwa 17:5

h Mwa 22:10-12

i Mwa 15:18

j Kut 2:23-25
Kut 3:7

nyingine ya siku walikuwa wakiungama na kumwinamia Yehova Mungu wao.

4 Yeshua, Bani, Kadmieli, Shebania, Buni, Sherebia,^a Bani, na Kenani wakasimama kwenye jukwaa^b la Walawi na kumlilia Yehova Mungu wao kwa sauti kubwa. **5** Nao Walawi, yaani, Yeshua, Kadmieli, Bani, Hashabneya, Sherebia, Hodia, Shebania, na Pethahia wakasema: “Simameni, msifuni Yehova Mungu wenu kwa umilele wote.*^c Na walisifu jina lako tukufu, ambalo limekwezwa juu kuliko baraka zote na sifa zote.

6 “Wewe peke yako ndiye Yehova;^d uliumba mbingu, naam, mbingu za mbingu na jeshi lake lote, dunia na vyote vilivyo juu yake, bahari na vyote vilivyomo. Nawe unavihifadhi vyote hai, na jeshi la mbinguni linakuinamia wewe. **7** Wewe ndiye Yehova Mungu wa kweli, uliyemchagua Abramu,^e ukamtoa katika jiji la Uru^f la Wakaldayo na ukampa jina Abrahamu.^g **8** Nawe ukaona moyo wake ukiwa mwaminifu mbele zako;^h basi ukafanya agano naye ili umpe nchi ya Wakanaani, Wahiti, Waamori, Waperizi, Wayebusi, na Wagirgashi, ili kuupa uzao wake* nchi hiyo;ⁱ nawe ukatimiza ahadi zako, kwa maana wewe ni mwadilifu.

9 “Basi ukaona mateso ya mababu zetu huko Misri,^j nawe ukasikia kilio chao kwenye Bahari Nyekundu. **10** Kisha ukafanya ishara na miujiza dhidi ya Farao na wa-

9:5 *Au “milele hata milele.” 9:8 *Tnn., “mbegu yake.”

tumishi wake wote na watu wote wa nchi yake,^a kwa maana ulijua waliwatendea kwa kimbelembele.^b Ukajijengea jina ambalo limedumu hadi leo hii.^c **11** Nawe ukaitengani bahari mbele yao, waka-vuka bahari juu ya nchi kavu,^d na wale waliowafuatia ukawatupa ndani ya maji mengi kama vile jiwe linavyotupwa ndani ya bahari iliyo chafuka.^e **12** Uliwaongoza mchana kwa nguzo ya wingu, na usiku kwa nguzo ya moto, ili kuwaangazia njia waliyopaswa kupitia.^f **13** Nawe ukashuka kwenye Mlima Sinai^g ukazunguma nao kutoka mbinguni^h na kuwapa hukumu za uadilifu, sheria za kweli,^{*} masharti bora na amri bora.ⁱ **14** Ukawajulisha Sabato yako takatifu/ na kuwapa amri, masharti, na sheria kupitia Musa mtumishi wako. **15** Walipokuwa na njaa uliwapa mkate kutoka mbinguni,^k walipokuwa na kiu ukawapa maji kutoka kwenye mwamba,^l na ukawaambia waingie na kuimiliki nchi ambayo ulikuwa umeapa* kwamba utawapatia.

16 "Lakini mababu zetu, wakatenda kwa kimbelembele^m na kuwa wakaidi,^{*n} nao hawakusikiliza amri zako. **17** Walikataa kusikiliza^o wala hawakukumbuka matendo yako ya ajabu uliyofanya miongoni mwao, lakini wakawa wakaidi,^{*} nao wakachagua kiongozi ili warudi Misri ambako walikuwa watumwa.^p

9:13 *Au "sheria zinazotegemeka."

9:15 *Tnn., "uliinua mkono wako."

9:16 *Tnn., "na kufanya shingo yao kuwa ngumu." 9:17 *Tnn., "wakafanya shingo yao kuwa ngumu."

SURA YA 9

a Kut 7:3

Kum 6:22

b Kut 5:2

c Kut 9:16

d Kut 14:21, 22

e Kut 15:1, 5, 10

f Kut 13:21

Kut 14:19, 20

g Kut 19:11

h Kum 4:10, 36

i Kum 4:8

j Kut 16:29

Kut 20:8-11

Kum 5:12-14

k Kut 16:4

l Kut 17:6

m Hes 14:44

n Kum 9:6

o Hes 14:11, 41

p Hes 14:1, 4

Safu ya 2

a Kut 34:6

Hes 14:18

b Kum 4:31

c Kut 32:1, 4

d Hes 14:19, 20

e Kut 40:38

Hes 9:15

f Hes 11:17, 25

g Kut 16:14, 15

h Hes 20:8

i Kut 16:35

Hes 14:33

Kum 2:7

j Kum 29:5

k Yos 11:23

l Hes 21:23, 24

Kum 2:31

m Hes 21:26

n Hes 21:33, 35

o Mwa 15:1, 5

p Mwa 12:7

Mwa 26:3

q Hes 14:29-31

Yos 21:43

r Yos 18:1

Lakini wewe ni Mungu uliye tayari kusamehe,^{*} mwenye huruma[#] na rehema, usiye mwepesi wa hasira, una upendo mwingi mshikamani-fu,^{Δa} nawe hukuwaacha.^b **18** Hata walipojitengezea sanamu ya ndama wa chuma^{*} na kusema, 'Huyu ndiye Mungu wenu aliyewaongoza kutoka Misri,^c nao wakatenda matendo makubwa ya ukosefu wa heshima, **19** hata wakati huo, kwa rehema zako nyingi, hukuwaacha nyikani.^d Nguzo ya wingu iliyowaongoza njiani mchana haikuondoka juu yao, wala nguzo ya moto iliyowaangazia njia usiku.^e **20** Nawe ukawapa roho yako njema ili iwape ufahamu,^f hukuwanyima mana vinywani mwao,^g na walipohisi kiu ukawapa maji.^h **21** Kwa miaka 40 uliwapa chakula nyikani.ⁱ Hawakukosa chochote. Mavazi yao hayakuchakaa,^j wala miguu yao haikuvimba.

22 "Uliwapa falme na mataifa, ukawagawia kipande kwa kipande.^k nao wakamiliki nchi ya Sihoni,^l yaani, nchi ya mfalme wa Heshboni,^m na pia nchi ya Oguⁿ mfalme wa Bashani. **23** Nawe ukawafanya wana wao kuwa wengi kama nyota za mbinguni.^o Kisha ukawaleta katika nchi ambayo ulikuwa umewaahidi mababu zao kwamba wanapaswa kuingia na kuimiliki.^p **24** Basi wana wao wakaingia na kuimiliki nchi hiyo,^q nawe ukawatiisha Wakanaani waliioishi katika nchi hiyo,^r

9:17 *Au "Mungu mwenye matendo ya kusamehe." [#]Au "neema." ^ΔAu "fadhili nyingi zenye upendo." 9:18 *Au "sanamu ya kuyeyushwa."

ukawatia mikononi mwao, wao pamoja na wafalme wao na wakaaji wa nchi, ili wawatendee wapendavyo. **25** Wakateka majiji yenye ngome^a na ardhi yenye rutuba,^{*b} wakamiliki nyumba zilizojaa vitu vyema vya kila aina, visima ambavyo tayari vilikuwa vimchimbwa, mashamba ya mizabibu, mizeituni,^c na miti ya matunda kwa wingi. Hivyo wakala na kushiba na kunenepa, nao wakaufurahia wema wako mwingi.

26 "Hata hivyo, hawakutii, bali walikuasi^d na kuigeuzia mgongo Sheria yako.* Wakawau manabii wako walioawanya wakurudie, nao wakatenda matendo maku-bwa ya ukosefu wa heshima.^e **27** Kwa sababu hiyo uliwatia mikononi mwa maadui wao,^f walioendelea kuwatesa.^g Lakini walipokuwa wakiteseka walikulilia, nawe uliwasikia ukiwa mbinguni; na kwa sababu ya rehema zako nyingi, uli-wapa waokozi waliowaoko kutoka mikononi mwa maadui wao.^h

28 "Lakini mara tu walipopata utulivu, walitenda tena yaliyo maovu mbele zako,ⁱ nawe ulikuwa ukiwaacha mikononi mwa maadui wao, ambao waliwakandamiza.*^j Kisha walirudi na kukuomba msaada,^k nawe uliwasikiliza ukiwa mbinguni na kuwaoko tena na tena kwa sababu ya rehema zako nyingi.^l **29** Ingawa uliwaonya ili wairudie Sheria yako, walitenda kwa kimbelebele na kuka-

9:25, 35 *Au "iliyonona." 9:26 *Tnn., "kuitupa Sheria yako nyuma yao." 9:28 *Au "waliwaponda."

SURA YA 9

a Kum 3:4, 5

b Kum 8:7-9

c Yos 24:13

d Kum 31:20
Kum 32:15
Amu 2:12e 2Fa 21:11
Zb 106:38

f Amu 2:14

g Kum 31:17

h Amu 2:18
Amu 3:9, 15
1Sa 12:11
2Fa 13:4, 5

i Amu 2:19

j Amu 4:1, 2
Amu 6:1

k Amu 6:6

l Zb 106:43-45

Safu ya 2

a 2Fa 17:13, 14
2Nya 24:19

b Law 18:5

c Ro 10:21

d 2Nya 36:15, 16
Isa 42:24
Yer 40:2, 3

e Eze 14:22

f Kut 34:6
Kum 4:31g Kum 7:9
Da 9:4

h 2Fa 24:12, 14

i Yer 34:18-20

j Omb 4:13, 14

k 2Fa 17:6

l Da 9:5

m Kum 28:47
Kum 32:15

taa kusikiliza amri zako;^a nao wakatenda dhambi kwa kutofuata masharti yako, ambayo mtu akiyafuata ataishi.^b Lakini walikugeuzia mgongo na kufanya shingo zao ziwe ngumu, nao wakakataa kukusikiliza. **30** Uliwaonyesha subira^c kwa miaka mingi na ukandelea kuwaonya kwa roho yako kupitia manabii wako, lakini walikataa kusikiliza. Mwishowe ukawatia mikononi mwa mataifa ya nchi hizo.^d

31 Na kwa sababu ya rehema zako nyingi, hukuwaangamiza^e wala kuwaacha, kwa maana wewe ni Mungu mwenye huruma* na rehema.^f

32 "Na sasa, Ee Mungu wetu, Mungu mkuu, mwenye nguvu, mwenye kuogopesha, unayeshika agano lako na kutenda kwa upendo mshikamanifu,^g usiyaone kuwa madogo mateso yote yaliyotupata sisi, wafalme wetu, wakuu wetu,^h makuhani wetu,ⁱ manabii wetu,^j mababu zetu, na watu wako wote tangu siku za wafalme wa Ashuru^k mpaka leo hii. **33** Umekuwa mwadilifu katika mambo yote yaliyotupata, kwa maana umetenda kwa uaminifu; lakini ni sisi tuli-totenda uovu.^l **34** Wafalme wetu, wakuu wetu, makuhani wetu, na mababu zetu hawajashika Sheria yako wala kusikiliza amri zako wala vikumbusho ulivyowapa* ili kuwaonya. **35** Hata walipokuwa kwenye ufalme wao wakifurahia wema mwingi uliowapa na katika nchi kubwa na yenye rutuba* uliyowapa, hawakukutumikia^m wala kuacha mazoea

9:31 *Au "neema." 9:34 *Au "maonyo uliyowapa."

yao maovu. **36** Basi leo hii sisi ni watumwa^a—naam, watumwa katika nchi ambayo uli-wapa mababu zetu ili wale matunda yake na vitu vyake vye-ma. **37** Mazao yake mengi ni ya wafalme uliowafanya watutawale kwa sababu ya dhambi zetu.^b Wanatutawala wependavyo na kuitendea mifugo yetu wapendavyo, tunate-seka sana.

38 “Basi kwa sababu ya hayo yote, tunafanya mapatano thabiti^c kwa maandishi, nayo yamethibitishwa kwa muhuri wa wakuu wetu, Walawi wetu, na makuhani wetu.”^d

10 Wale walioyathibitisha kwa kutia muhuri^e walikuwa:

Gavana* Nehemia, mwana wa Hakalia,

Na Sedekia, **2** Seraya, Azaria, Yeremia, **3** Pashuri, Amaria, Malkiya, **4** Hatushi, Shebania, Maluku, **5** Harimu,^f Meremothi, Obadia, **6** Danieli,^g Ginethoni, Baruku, **7** Meshulamu, Abiya, Miyamini, **8** Maazia, Bilgai, na Shemaya; hao ndio makuhani.

9 Pia Walawi: Yeshua mwana wa Azania, Binui wa wana wa Henadadi, Kadmieli,^h **10** na ndugu zao Shebania, Hodia, Kelita, Pelaya, Hanani, **11** Mika, Rehobu, Hashabia, **12** Zakuri, Sherebia,ⁱ Shebania, **13** Hodia, Bani, na Beninu.

14 Viongozi wa watu: Paroshi, Pahath-moabu,^j Elamu, Zatu, Bani, **15** Buni, Azgadi, Bebai, **16** Adoniya, Bigvai, Adini, **17** Ate-

10:1 *Au “Tirshatha,” cheo cha Kiajemi cha gavana wa mkoa.

SURA YA 9

a Kum 28:48
Ezr 9:9

b Kum 28:15, 33
Ne 5:4

c 2Fa 23:3
2Nya 15:12
Ezr 10:3

d Ne 10:28, 29

SURA YA 10

e Ne 9:38

f Ezr 2:1, 39

g Ezr 8:1, 2

h Ezr 3:9
Ne 12:8

i Ne 12:24

j Ne 7:6, 11

Safu ya 2

a Ne 8:1
Ne 9:2

b Kut 34:15, 16
Kum 7:3, 4

c Kut 20:10

d Kut 12:16
Hes 29:1, 12

e Kut 23:10, 11
Law 25:4, 5

f Kum 15:1-3

ri, Hezekia, Azuri, **18** Hodia, Hashumu, Besai, **19** Harifu, Anathothi, Nebai, **20** Magpiashi, Meshulamu, Heziri, **21** Meshezabeli, Sadoki, Yadua, **22** Pelatia, Hanani, Anaya, **23** Hoshea, Hanania, Hashubu, **24** Haloheshi, Pilha, Shobeki, **25** Rehumu, Hashabna, Maaseya, **26** Ahiya, Hanani, Anani, **27** Maluku, Harimu, na Baana.

28 Watu wengine wote—makuhani, Walawi, walinzi wa malango, waimbaji, watumishi wa hekaluni,* kila mtu aliyejitenga na mataifa yaliyokuwa nchini ili afuate Sheria ya Mungu wa kweli,^a pamoja na wake zao, wana wao, na mabinti wao, kila mtu mwenye ujuzi na uelewaji[#]— **29** wakajiunga na ndugu zao, wakuu wao, wakajifunga kwa kiapo na laana, kwamba watate-mbea katika Sheria ya Mungu wa kweli, iliyotolewa kupitia Musa mtumishi wa Mungu wa kweli, na kufuata kwa maki-ni amri zote za Yehova Bwana wetu, hukumu zake, na masharti yake. **30** Hatutakubali mabinti wetu waolewe na watu wa mataifa yaliyo nchini, wala hatutakubali wana wetu wawaaoe mabinti wao.^b

31 Ikiwa watu wa mataifa hayo wataleta bidhaa zao na kila aina ya nafaka ili watuu-zie katika siku ya Sabato, hatutanunua chochote kutoka kwao siku ya Sabato^c au siku nyingine takatifu.^d Pia, mwaka wa saba^e hatutalima mashamba na tutayafuta madeni yote.^f

10:28 *Au “Wanethini.” Tnn., “waliotole-wa.” # Au labda, “wote wenye umri wa kutosha kuelewa.”

32 Pia, tukajiwekea wajibu kwamba kila mmoja wetu atoe sehemu ya tatu ya shekeli* kila mwaka kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya^a Mungu wetu,^a **33** kwa ajili ya mkate wa tabaka,^b toleo la nafaka la kila siku,^c dhahibu za kawaida za kuteketezwa za Sabato^d na miezi mipya,^e na kwa ajili ya sherehe rasmi,^f kwa ajili ya vitu vitakatifu, kwa ajili ya dhahibu za dhambi^g ili kufunika dhambi za Waisraeli, na kwa ajili ya kazi zote za nyumba ya Mungu wetu.

34 Pia, tukapiga kura ili kupanga wakati ambao kila ukoo* wa makuhani, Walawi, na watu wangeleta kuni kwenye nyumba ya Mungu wetu wakati uliowekwa, mwaka baada ya mwaka, ili kuwasha moto kwenye madhabahu ya Yehova Mungu wetu, kama ilivyoandikwa katika Sheria.^h **35** Pia tutaleta kwenye nyumba ya Yehova mazao ya kwanza yaliyokomaa ya nchi yetu na matunda ya kwanza yaliyoiva ya kila mti wa matunda, mwaka baada ya mwaka,ⁱ **36** vilevile tutatoa wazaliwa wetu wa kwanza wa kiume na pia wa mifugo yetu—kama ilivyoandikwa katika Sheria^j—wazaliwa wetu wa kwanza wa ng'ombe na wa kondoo. Tutawaleta kwenye nyumba ya Mungu wetu, kwa makuhani wanaohudumu kwenye nyumba ya Mungu wetu.^k **37** Pia, unga wetu wa kwanza ambao hau-

10:32 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14. ^aAu "hekalu la." 10:33 *Yaani, mkate wa wonyesho. 10:34 *Yaani, ukoo wa upande wa baba.

SURA YA 10

- a Kut 30:13
- b Law 24:5-7
- c Kut 29:40, 41
- d Hes 28:9
- e Hes 28:11-13
1Nya 23:31
- f Kum 16:16
- g Law 16:15
- h Law 1:7
Law 6:12, 13
- i Kut 23:19
Hes 18:8, 13
Kum 26:2
- j Kut 13:2
Hes 18:15
- k Hes 18:8, 11
1Ko 9:13

Safu ya 2

- a Hes 15:20
- b Law 27:30
- c Hes 18:8, 12
Kum 18:1, 4
- d 2Nya 31:11
- e Hes 18:21
- f Hes 18:26
- g Kum 12:5, 6
- h Kum 14:23
- i Ne 13:10, 11

SURA YA 11

- j Ne 7:4
- k Met 16:33

jakoblewa,^a michango yetu, matunda ya mti wa kila aina,^b divai mpya, na mafuta,^c tuta-wapelekea makuhani kwenye maghala* ya nyumba ya Mungu wetu,^d pia tutawapa Walawi sehemu ya kumi ya mazao ya mashamba yetu,^e kwa maana Walawi ndio wanaokusanya sehemu za kumi za mazao katika miji yetu yote ya kilimo.

38 Na kuhani, mwana wa Haruni, anapaswa kuwa pamoja na Walawi wanapokusanya sehemu ya kumi; Walawi nao wanapaswa kuleta sehemu ya kumi ya ile sehemu ya kumi katika nyumba ya Mungu wetu,^f kwenye vyumba vya* ghala. **39** Kwa maana Waisraeli na Walawi wanapaswa kuleta mchango^g wa nafaka, divai mpya, na mafuta^h kwenye maghala,* ambamo mna vyombo vya mahali patakatifu, na pia walinzi wa malango, waimbaji, na makuhani wanaohudumu. Hatutaipuza nyumba ya Mungu wetu.ⁱ

11 Sasa wakuu wa watu walikuwa wakiishi Yerusalemu;^j lakini watu wengine wote walipiga kura^k ili mtu mmoja kati ya watu kumi aishi Yerusalemu, lile jiji takatifu, na wale wengine tisa waliishi katika majiji mengine. **2** Isitoshe, watu waliwabariki wote waliojitolea kuishi Yerusalemu.

3 Na hawa ndio viongozi wa mkoa* walioishi Yerusalemu. (Waisraeli wengine wote, makuhani, Walawi, watumishi wa

10:37, 39 *Au "majumba ya kulia chakula." 10:38 *Au "majumba ya kulia chakula ya." 11:3 *Au "wilaya ya utawala."

hekaluni,^{*a} na wana wa watumishi wa Sulemani,^b waliishi katika majiji mengine ya Yuda, kila mmoja katika sehemu aliyomiliki jijini.^c

4 Pia, baadhi ya watu wa Yuda na Benjamini waliishi Yerusalemu.) Kati ya watu wa Yuda kulikuwa na Athaya mwana wa Uzia mwana wa Zekaria mwana wa Amaria mwana wa Shefatia mwana wa Mahalaleli wa wana wa Perezi,^d **5** na Maaseya mwana wa Baruku mwana wa Kolhoze mwana wa Hazaya mwana wa Adaya mwana wa Yoyaribu mwana wa Zekaria mwana wa Mshela. **6** Wana wote wa Perezi walioishi Yerusalemu walikuwa wanaume mashujaa 468.

7 Hawa ndio waliokuwa watu wa Benjamini: Salu^e mwana wa Meshulamu mwana wa Yoedi mwana wa Pedaya mwana wa Kolaya mwana wa Maaseya mwana wa Ithieli mwana wa Yeshaya, **8** na baada yake Gabai na Salai, watu 928; **9** na Yoeli mwana wa Zikri alikuwa msimamizi wao, na Yuda mwana wa Hase-nua alikuwa wa pili katika usimamizi wa jiji.

10 Kutoka kwa makuhani: Yedaya mwana wa Yoyaribu, Yakini,^f **11** Seraya mwana wa Hilikia mwana wa Meshulamu mwana wa Sadoki mwana wa Merayothi mwana wa Ahitubu,^g kiongozi wa nyumba ya* Mungu wa kweli; **12** na ndugu zao waliofanya kazi ya ile nyumba, watu 822; na Adaya mwana wa Yerohamu mwana wa Pelalia mwana

11:3, 21 *Au "Wanethini." Tnn., "waliolewa." 11:11 *Au "hekalu la."

SURA YA 11

a Yos 9:3, 27
Ezr 8:17

b Ezr 2:58

c Ezr 2:70

d Hes 26:20

e 1Nya 9:3, 7

f 1Nya 9:10-13

g 1Nya 6:12

Safu ya 2

a Yer 21:1, 2
Yer 38:1

b 1Nya 9:2, 14

c Ezr 10:14, 15

d Ezr 8:33
Ne 8:7

e Ne 11:22
Ne 12:25

f Ne 7:6, 44

g 1Nya 16:4
2Nya 5:13

h 1Nya 16:41, 42
2Nya 35:15

i 1Nya 9:2, 17
Ezr 2:1, 42
Ne 12:25

j Ezr 2:1, 58

k 2Nya 27:1, 3
Ne 3:26

wa Amzi mwana wa Zekaria mwana wa Pashuri^a mwana wa Malkiya, **13** na ndugu zake, viongozi wa koo,* watu 242, na Amashisai mwana wa Azareli mwana wa Azai mwana wa Meshilemothi mwana wa Imeri, **14** na ndugu zao 128 waliokuwa wanaume hodari na jasiri; na msimamizi wao alikuwa Zabdieli, aliyetoka katika familia mashuhuri.

15 Na kutoka kwa Walawi: Shemaya^b mwana wa Hashubu mwana wa Azrikamu mwana wa Hashabia mwana wa Buni, **16** na Shabethai^c na Yozabadi,^d wa viongozi wa Walawi, waliosimamia kazi za nje ya nyumba ya Mungu wa kweli; **17** na Matania,^e mwana wa Mika mwana wa Zabdi mwana wa Asafu,^f kiongozi wa waimbaji, aliyeongoza sifa wakati wa sala,^g na Bakbukia, wa pili kati ya ndugu zake, na Abda mwana wa Shama mwana wa Galali mwana wa Yeduthuni.^h **18** Walawi wote katika jiji takatifu walikuwa 284.

19 Na walenzi wa malango walikuwa Akubu, Talmoni,ⁱ na ndugu zao waliolinda malango walikuwa 172.

20 Waisraeli wengine wote, makuhani, na Walawi walikuwa katika majiji mengine yote ya Yuda, kila mmoja katika eneo alilorithi.* **21** Watumishi wa hekaluni^{*j} walikuwa wakiishi Ofeli,^k nao Siha na Gishpa waliwasimamia watumishi wa hekaluni.*

22 Msimamizi wa Walawi walioishi Yerusalemu alikuwa Uzi mwana wa Bani mwana

11:13 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 11:20 *Au "urithi wake mwenyewe."

wa Hashabia mwana wa Matania^a mwana wa Mika, wa wana wa Asafu, waimbaji; alisimamia kazi ya nyumba ya Mungu wa kweli. **23** Kwa maana mfalme alikuwa ametoa amri kwa ajili ya waimbaji,^b na kuli kuwa na mpango hususa kuhusu mahitaji yao ya kila siku. **24** Na Pethahia mwana wa Meshezabeli wa wana wa Zera mwana wa Yuda alikuwa mshauri wa mfalme* katika kila jambo lililowahusu watu.

25 Kuhusu maeneo na mashamba yake, baadhi ya watu wa Yuda waliishi Kiriath-arba^c na miji yake, Diboni na miji yake, Yekabzeeli^d na vijiji vyake, **26** huko Yeshua, Molada,^e Beth-peleti,^f **27** Hasarsuali,^g Beer-sheba na miji yake, **28** Siklagi,^h Mekona na miji yake, **29** En-rimoni,ⁱ Sora,^j na Yarmuthi, **30** Zanoa,^k Adulamu na vijiji vyake, Lakishi^l na mashamba yake, na huko Azeka^m na miji yake. Waliishi* kuanzia Beer-sheba mpaka Bonde la Hinomu.ⁿ

31 Na watu wa Benjamine waliishi Geba,^o Mikmashi, Aiya, Betheli^p na miji yake, **32** Anathothi,^q Nobu,^r Ananiya, **33** Hasori, Rama,^s Gitaimu, **34** Hadidi, Seboimu, Nebalati, **35** Lodi, na Ono,^t bonde la mafundi. **36** Na baadhi ya vikundi vya Walawi kutoka Yuda waliishi katikane eno la Benjamine.

12 Hawa ndio makuhani na Walawi waliopanda kwenda na Zerubabeli^u mwana wa Shealtieli,^v na Yeshua;^w Seraya, Yeremia, Ezra,

11:24 *Tnn., "alikuwa kwenye mkono wa mfalme." 11:30 *Au "Walipiga kambi."

SURA YA 11

- a 1Nya 9:2, 15
- b Ezr 6:3, 9
Ezr 7:21-24
- c Mwa 23:2
Yos 14:15
- d Yos 15:21
2Sa 23:20
- e Yos 15:21, 26
Yos 19:1, 2
- f Yos 15:21, 27
- g Yos 19:1, 3
- h Yos 15:21, 31
Yos 19:1, 5
1Sa 27:5, 6
- i Yos 15:21, 32
- j Yos 15:20, 33
Yos 19:40, 41
- k Yos 15:20, 34
Ne 3:13
- l Yos 15:20, 39
Isa 37:8
- m Yos 15:20, 35
- n Yos 15:8, 12
2Fa 23:10
- o Yos 18:21, 24
- p Mwa 28:19
Yos 18:11, 13
- q Yos 21:8, 18
- r 1Sa 21:1
- s Yos 18:21, 25
- t 1Nya 8:12
Ezr 2:1, 33

SURA YA 12

- u Ezr 1:8, 11
- v Mt 1:12
- w Zek 3:1

Safu ya 2

- a Ezr 2:1, 40
Ezr 3:9
- b 1Nya 9:2, 15
Ne 11:17
Ne 12:25
- c Ne 3:1
- d Ne 13:28
- e Ne 11:3, 11
- f Ne 12:1
- g Ezr 2:1, 39
- h Ne 12:1, 4
- i Ne 12:1, 5
- j Ne 12:1, 6

2 Amaria, Maluku, Hatushi, **3** Shekania, Rehumu, Mere-mothi, **4** Ido, Ginethoi, Abiya, **5** Miyamini, Maadia, Bilga, **6** Shemaya, Yoyaribu, Yedaya, **7** Salu, Amoki, Hilkaia, na Yedaya. Hao ndio waliokuwa viongozi wa makuhani na ndugu zao katika siku za Yeshua.

8 Walawi walikuwa Yeshua, Binui, Kadmieli,^a Sherebia, Yuda, na Matania^b aliyeongozwa uimbaji wa nyimbo za shukrani akiwa pamoja na ndugu zake. **9** Walisimama wakitazamana na ndugu zao Bakbukia na Uni wakati wa zamu za kulinda.* **10** Yeshua alimzaa Yoyakimu, Yoyakimu alimzaa Eliashibu,^c naye Eliashibu alimzaa Yoyada.^d **11** Naye Yoyada alimzaa Yonathani, naye Yonathani akamzaa Yadaa.

12 Katika siku za Yoyakimu, hawa ndio waliokuwa makuhani, viongozi wa koo:* wa Seraya,^e Meraya; wa Yeremia, Hanania; **13** wa Ezra,^f Meshulamu; wa Amaria, Yehohanani; **14** wa Maluki, Yonathani; wa Shebania, Yosefu; **15** wa Harimu,^g Adna; wa Merayothi, Helkai; **16** wa Ido, Zekaria; wa Ginethoni, Meshulamu; **17** wa Abiya,^h Zikiri; wa Miniamini, . . . ;* wa Moadia, Piltai; **18** wa Bilga,ⁱ Shamua; wa Shemaya, Yehonathani; **19** wa Yoyaribu, Matenai; wa Yedaya,^j Uzi; **20** wa Salai, Kalai; wa Amoki, Eberi; **21** wa Hil-

12:9 *Au labda, "wakati wa utumishi." 12:12 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 12:17 *Inaonekana jina fulani limeondolewa hapa katika maandishi ya Kiebrania.

kia, Hashabia; wa Yedaya, Nethaneli.

22 Viongozi wa koo* za Walawi na za makuhani katika siku za Eliashibu, Yoyada, Yohanani, na Yadua^a waliandikishwa, vilevile makuhani, mpaka wakati wa ufalme wa Dario Mwajemi.

23 Walawi waliokuwa viongozi wa koo* waliandikishwa katika kitabu cha historia ya nyakati, mpaka siku za Yohanani mwana wa Eliashibu. **24** Viongozi wa Walawi walikuwa Hashabia, She-rebia, na Yeshua^b mwana wa Kadmieli,^c na ndugu zao walisisimama wakitazamana walipokuwa wakiimba sifa na kumshukuru Mungu kulingana na maagizo ya Daudi^d mtu wa Mungu wa kweli, kikundi cha ulinzi kwa kikundi cha ulinzi. **25** Matania,^e Bakbukia, Obadia, Meshulamu, Talmoni, na Akubu^f walikuwa walinzi wa malango,^g walilinda maghala yaliyokuwa karibu na malango. **26** Hao walitumikia katika siku za Yoyakimu mwana wa Yeshua^h mwana wa Yozadaki na katika siku za gavana Nehemia na Ezraⁱ aliye-kuwa kuhani na mwandishi.*

27 Wakati wa kuzindua kuta za Yerusalemu, Walawi walitafutwa kila mahali walipokuwa ili waje Yerusalemu kusherehekea uzinduzi kwa kushangilia, kwa nyimbo za shukrani,^j na kwa matoazi, vinanda, na vinubi. **28** Na wana wa waimbaji* wakakusanyika pamoja kutoka kati-

12:22, 23 *Yaani, ukoo wa upande wa baba. 12:26, 36 *Au "aliyenakili maandishi." 12:28 *Au "Na waimbaji waliozoezwa."

SURA YA 12

a Ne 12:10, 11

b Ne 8:7

c Ezr 2:1, 40

d 1Nya 16:4
1Nya 23:28, 30

e 1Nya 9:2, 15

f 1Nya 9:17
Ezr 2:1, 42
Ne 11:1, 19

g 1Nya 9:22-27

h Ezr 3:2, 8

i Ezr 7:1, 6

j 2Nya 5:13
2Nya 7:6

Safu ya 2

a 1Nya 2:54
1Nya 9:2, 16
Ne 7:6, 26

b Yos 15:7, 12

c Yos 21:8, 17
Ne 11:31

d Ezr 2:1, 24

e Kut 19:10

f Ne 7:1

g Ne 6:15

h Ne 2:13
Ne 3:13i Hes 10:2
2Nya 5:12

j 1Nya 25:1, 2

k 1Nya 23:5

l Ne 8:4

m Ne 2:14

n Ne 3:15

o 2Sa 5:7, 9

p Ne 3:26
Ne 8:1

ka wilaya,* kutoka maeneo yaliyokuwa karibu na Yerusalemu, na kutoka vijiji vya Wanetofa,^a **29** kutoka Bethgilgali,^b na kutoka mashamba ya Geba^c na Azmavethi,^d kwa maana waimbaji walikuwa wamejiingee vijiji kuzunguka Yerusalemu. **30** Na makuhani na Walawi wakajitakasa na kuwatakasa watu,^e malango,^f na ukuta.^g

31 Kisha nikawaleta wakuu wa Yuda juu wa ukuta. Nikapanga makundi mawili makubwa yaliyoimba nyimbo za shukrani na vikundi vya kuwafuata, kikundi kimoja kilienda upande wa kulia wa ukuta kuelekea Lango la Marundo ya Majivu.^h **32** Hoshaya na nusu ya wakuu wa Yuda walitembea nyuma yao, **33** pamoja na Azaria, Ezra, Meshulamu, **34** Yuda, Benjamini, Shemaya, na Yeremia. **35** Walikuwa pamoja na baadhi ya wana wa makuhani waliokuwa na tarumbeta:ⁱ Zekaria mwana wa Yonathani mwana wa Shemaya mwana wa Matania mwana wa Mikaya mwana wa Zakuri mwana wa Asafu,^j **36** na ndugu zake Shemaya, Azareli, Milalai, Gilalai, Maai, Nethaneli, Yuda, na Hanani, wakiwa na vyombo vya muziki vya Daudi^k mtu wa Mungu wa kweli; na Ezra^l mwandishi* akawatangulia. **37** Kwenye Lango la Chemchemi^m walipanda moja kwa moja Ngaziⁿ ya Jiji la Daudi^o kupitia njia inayopanda kwenye ukuta juu ya Nyumba ya Daudi mpaka kwenye Lango la Maji^p upande wa mashariki.

12:28 *Yaani, wilaya iliyozunguka Yordani.

38 Kundi la pili lililoimba nyimbo za shukrani lilitembea kuelekea kushoto,* nami nikalifuata pamoja na nusu ya watu, juu ya ukuta kwenye Mnara wa Majiko ya Kuokea^a mpaka kwenye Ukuta Mpana^b **39** na kupita juu ya Lango la Efraimu^c na juu ya Lango la Jiji la Kale^d mpaka kwenye Lango la Samaki,^e Mnara wa Hananeli,^f Mnara wa Mea, na mpaka kwenye Lango la Kondoo;^g kisha wakasimama kwenye Lango la Mlinzi.

40 Mwishowe yale makundi mawili yaliyoimba nyimbo za shukrani yakasimama mbele ya nyumba ya Mungu wa kweli; mimi pia nikasimama pamoja na nusu ya watawala wa-saidizi waliokuwa pamoja nami, **41** na makuhani Elia-kimu, Maaseya, Miniamani, Mikaya, Elioenai, Zekaria, na Hanania, wakiwa na tarumbeta, **42** na Maaseya, Shemaya, Eleazari, Uzi, Yehohanani, Malkiya, Elamu, na Ezeri. Na waimbaji hao wakaimba kwa sauti kubwa wakiongozwa na Izrahia.

43 Siku hiyo walitoa dhabihu nyingi na kushangilia,^h kwa maana Mungu wa kweli aliwafanya washangilie kwa shangwe kubwa. Wanawake na watoto wakashangilia pia,ⁱ hivi kwamba sauti za kushangilia jijini Yerusalemu zikasingilia mbali sana.^j

44 Siku hiyo wanaume waliwekwa ili kusimamia maghala^k ya michango,^l mazao ya kwanza,^m na sehemu za kumi.ⁿ Kutoka katika mashamba ya majiji walipaswa kukusanya

SURA YA 12

a Ne 3:11

b Ne 3:8

c 2Fa 14:13
Ne 8:16

d Ne 3:6

e 2Nya 33:14
Ne 3:3f Yer 31:38
Zek 14:10g Ne 3:1
Yoh 5:2

h Ezz 6:16, 17

i Yer 31:13

j Ezz 3:10, 13

k 2Nya 31:11

l Ne 10:39

m Ne 10:35-37

n Ne 10:38
Ne 13:12, 13

Safu ya 2

a Kut 34:26
Hes 15:18, 19
Kum 26:2

b Hes 18:21

c 1Nya 25:1, 6

d Ezz 3:2
Hag 1:12
Lu 3:23, 27

e Ne 11:23

f Ne 10:39

g Hes 18:21

SURA YA 13

h Kum 31:11
Ne 8:2, 3
Mdo 15:21

i Mwa 19:36-38

j Kum 23:3, 6

k Hes 22:4-6

l Hes 23:8
Hes 24:10m Ezz 10:10, 11
Ne 9:1, 2

kwenye maghala hayo mafungu yaliyoamriwa na Sheria^a kwa ajili ya makuhani na Walawi,^b kwa maana kulikuwa na shangwe huko Yuda kwa sababu ya makuhani na Walawi waliokuwa wakihudumu. **45** Nao wakaanza kushughulikia majukumu waliyopewa na Mungu wao na kutimiza wajibu wa kutakasa, kama walivyofanya waimbaji na walinni wa malango, kulingana na maagizo ya Daudi na ya Sulemani mwanawe. **46** Kwa maana zamani za kale katika siku za Daudi na Asafu, kulikuwa na viongozi wa* waimbaji wa nyimbo za kumsifu na kumshukuru Mungu.^c **47** Na katika siku za Zerubabeli^d na siku za Nehemia, Waisraeli wote walitoa mafungu kwa ajili ya waimbaji^e na walinni wa malango,^f kulingana na uhitaji wa kila siku. Pia, waliweka kando fungu kwa ajili ya Walawi,^g na Walawi waliweka kando fungu kwa ajili ya wazao wa Haruni.

13 Siku hiyo kitabu cha Musa kilisomwa watu wote wakisikia,^h na wakaona imeandikwa kwamba Mwamoni au Mmoabuⁱ hapaswi kamwe kuingia katika kutaniko la Mungu wa kweli,^j **2** kwa maana hawakuwapokea Waisraeli kwa mkate na maji, badala yake walimkodi Balaa-mu ili awalaani.^k Hata hivyo, Mungu wetu aliigeuza laana hiyo kuwa baraka.^l **3** Mara tu waliposikia Sheria, wakaanza kuwatenga watu wote wenyewe asili ya kigeni* ili wasichangamane na Waisraeli.^m

12:46 *Tnn., "vichwa vya." 13:3 *Au "wenye asili mbalimbali."

4 Sasa kabla ya wakati huo, kuhani aliyesimamia maghala* ya nyumba ya[#] Mungu wetu^a alikuwa Eliashibu,^b mtu wa ukoo wa Tobia.^c 5 Alikuwa amempa ghala kubwa,* mahali ambapo zamani walipatumia kuweka toleo la nafaka, ubani, na vyombo na sehemu ya kumi ya nafaka, divai mpya, na mafuta,^d vitu ambavyo Walawi,^e waimbaji, na walini wa malango walipaswa kupewa, pamoja na michango kwa ajili ya makuhani.^f

6 Wakati huo wote mimi sikuwa Yerusalemu, kwa maana nilirudi kwa mfalme katika mwaka wa 32^g wa utawala wa Mfalme Artashasta^h wa Babiloni; na baada ya muda fulani nikamwomba mfalme ruhusa ya kuondoka. 7 Kisha nikafika Yerusalemu, nami nikao-na jambo baya sana ambalo Eliashibuⁱ alikuwa amefanya kwa kumpa Tobia^j ghala katika ua wa nyumba ya Mungu wa kweli. 8 Jambo hilo lilinikasirisha sana, basi nikavitupa nje ya ghala* vitu vyote vya nyumba ya Tobia. 9 Kisha nikatoa amri, nao wakayatakasa maghala,* nami nikavirudisha humo vyombo vya nyumba ya Mungu wa kweli,^k pamoja na toleo la nafaka na ubani.^l

10 Pia, nikagundua kwaamba Walawi^m hawakuwa wakipewa mafungu yao,ⁿ hivyo Walawi na waimbaji waliofanya kazi walikuwa wameondoka, kila mmoja akaenda kwenye shamba lake.^o 11 Basi nikawakemea watawala wasaidi-

13:4, 9 *Au "majumba ya kulia chakula." 13:4 #Au "hekalu la." 13:5, 8 *Au "jumba la kulia chakula."

SURA YA 13

a Ne 10:37, 38

b Ne 3:1

c Ne 2:10

d Kum 18:3, 4

e Hes 18:24

f Ne 12:44

g Ne 5:14

h Ezz 7:1
Ne 2:1

i Ne 12:10

j Ne 4:7

k Ne 10:39

l Law 2:14, 15

m Ne 10:37
Ne 12:47

n Mal 3:8

o Hes 35:2

Safu ya 2

a Ezz 9:2

b Ne 10:39

c Law 27:30
Hes 18:21

d Ne 10:38, 39
Mal 3:10

e Ne 5:19

f Ebr 6:10

g Kut 20:10
Kut 34:21
Kut 35:2

h Yer 17:21, 27

i Ne 10:31

zi^a na kuwauliza: "Kwa nini nyumba ya Mungu wa kweli imepuuzwa?"^b Kwa hiyo nikawakusanya na kuwarudisha kwenye kazi zao. 12 Na watu wote wa Yuda wakaleta kwenye maghala sehemu ya kumi^c ya nafaka, divai mpya, na mafuta.^d 13 Kisha nikawaweka kuhani Shelemia, Sadoki mwandishi,* na Pedaya aliye-kuwa Mlawi wasimamia maghala, na msaidizi wao alikuwa Hanani mwana wa Zakuri mwana wa Matania, kwa maana walionwa kuwa wanaume wenye kutegemeka. Walikuwa na jukumu la kuwagawia ndugu zao.

14 Unikumbuke mimi,^e Ee Mungu wangu, kuhusu jambo hili, nawe usiyafutilie mbali matendo yangu ya upe-ndo mshikamanifu ambayo nimetenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu na utumishi wake.*^f

15 Siku hizo niliwaona watu huko Yuda wakikanyaga mashinikizo ya divai siku ya Sabato,^g wakileta marundo ya nafaka na kuyapakia juu ya punda, wakileta divai, zabibu, tini, na kuingiza kila aina ya mzigo Yerusalemu siku ya Sabato.^h Basi nikawaonya wasiuzze bidhaa siku hiyo.* 16 Na Watiro walioishi jijini walikuwa wakileta samaki na bidhaa za kila aina na kuwauzia watu wa Yuda na Yerusalemu siku ya Sabato.ⁱ 17 Basi nikawakemea wakuu wa Yuda na kuwaambia: "Ni uovu gani huu mnaofanya, hata mnaitia unajisi siku

13:13 *Au "aliyenakili maandishi." 13:14 *Au "utunzaji wake." 13:15 *Au labda, "nikawaonya siku hiyo wasiuzze bidhaa."

ya Sabato? **18** Je, mababu zenu hawakufanya hivyo, hivi kwamba Mungu wetu akatuletea sisi na pia jiji letu msiba huu wote? Sasa mnazidisha hasira yake inayowaka dhidi ya Israeli kwa kuitia unajisi Sabato.”^a

19 Hivyo, mara tu vivuli vilipoanza kuangukia malango ya Yerusalemu kabla ya Sabato, niliamuru milango ifungwe. Pia niliwaambia kwamba hawapaswi kuifungua mpaka Sabato iishe, nami nikawaweka baadhi ya watumishi wangu mwenyewe malangoni ili mizigo yoyote isiingizwe siku ya Sabato. **20** Basi wafanyabiashara na wauzaji wa bidhaa za kila aina wakalala nje ya Yerusalemu mara moja au mbili. **21** Ndipo nikawaonya na kuwaambia: “Kwa nini mnalala mbele ya ukuta usiku? Mkifanya hivyo tena, nitawaondoa kwa nguvu.” Tangu wakati huo hawakuja tena siku ya Sabato.

22 Nikawaambia Walawi kwamba wanapaswa kujitakasa kwa ukawaida na kuja kulinda malango ili siku ya Sabato iendelee kuwa takatifu.^b Ee Mungu wangu, unikumbuke pia kwa jambo hili, na unihurumie kwa sababu ya upeendo wako mwingi mshikamanifu.^c

23 Siku hizo niliwaona pia Wayahudi waliokuwa wameoa* wanawake Waashdodi,^d Waamoni,^e na Wamoabu.^f **24** Nusu ya wana wao walizungumza Kiashdodi na nusu walizungumza lugha za mataifa mbalimbali, lakini haku-

13:23 *Au “wamewaingiza ndani ya nyumba zao.”

SURA YA 13

a Kut 20:8-10

b Kum 5:12

c Ne 5:19
Ne 13:14
Ne 13:30, 31

d Yos 13:2, 3

e Kum 23:3, 4

f Ezz 9:1, 2
Ezz 10:10
2Ko 6:14

Safu ya 2

a Kum 25:2
Ezz 7:26

b Kum 7:3, 4
Ne 10:30

c 1Fa 3:12, 13
2Nya 9:22

d 2Sa 12:24

e 1Fa 11:1-5

f Ezz 10:2

g Ne 12:10

h Ne 3:1
Ne 13:4

i Ne 2:10
Ne 6:14

j Kut 40:15
Hes 25:11-13

k Mal 2:4

l 1Nya 23:6
1Nya 25:1

m Ne 10:34

n Ne 5:19

na yeyote kati yao aliyejua kuzungumza lugha ya Wayahudi. **25** Ndipo nikawakemea na kuwalaani, nikawapiga baadhi ya wanaume hao,^a nikazing’oa nywele zao na kuwaapisha hivi kwa Mungu: “Msikubali mabinti wenu waolewe na wana wao, na msikubali mabinti wao waolewe na wana wenu au ninyi wenyewe.^b **26** Je, Mfalme Sulemani wa Israeli hakutenda dhambi kwa sababu yao? Haku kuwa na mfalme kama yeye miongoni mwa mataifa mngi;^c naye alipendwa na Mungu wake,^d hivi kwamba Mungu akamweka kuwa mfalme wa nchi yote ya Israeli. Lakini wake wa kigeni walimfanya hata yeye atende dhambi.^e **27** Je, si jambo linaloshangaza kwenu kutenda uovu huu mkubwa kwa kutokuwa waaminifu kwa Mungu wetu kwa kuoa wanawake wa kigeni?”^f

28 Mmoja wa wana wa Yoyada^g mwana wa kuhani mkuu Eliashibu^h alikuwa amemwoa binti ya Sanbalatiⁱ Mhoroni. Kwa hiyo nikamfukuza kutoka mbele yangu.

29 Wakumbuke, Ee Mungu wangu, kwa sababu wamechafua ukuhani na agano la ukuhani^j na pia Walawi.^k

30 Nami nikawatakasaa kutokana na uchafu wote wa kigeni, nami nikawapa makuhani na Walawi majukumu yao, kila mmoja katika utumishi wake,^l **31** nami nikapanga ili kuni^m ziletwe wakati unaofaa na pia mazao ya kwanza yaliyokomaa.

Unikumbuke na kunitendea wema,* Ee Mungu wangu.ⁿ

13:31 *Au “na kunipa kibali.”

ESTA

YALIYOMO

- | | |
|---|---|
| <p>1 Karamu ya Mfalme Ahasuero kule Shushani (1-9)
Malkia Vashti akataa kutii (10-12)
Mfalme ashauriana na wanaume wake wenye hekima (13-20)
Barua za agizo la mfalme zatumwa (21, 22)</p> <p>2 Malkia mpya atafutwa (1-14)
Esta awa malkia (15-20)
Mordekai afunua njama (21-23)</p> <p>3 Mfalme amkweza Hamani (1-4)
Hamani apanga njama ya kuwaangamiza Wayahudi (5-15)</p> <p>4 Mordekai aomboleza (1-5)
Mordekai amwomba Esta aingilie kati (6-17)</p> | <p>5 Esta aenda mbele ya mfalme (1-8)
Hasira na kiburi cha Hamani (9-14)</p> <p>6 Mordekai aheshimiwa na mfalme (1-14)</p> <p>7 Esta afunua uovu wa Hamani (1-6a)
Hamani atundikwa kwenye mti alioutengeneza (6b-10)</p> <p>8 Mordekai apandishwa cheo (1, 2)
Esta amsihi mfalme (3-6)
Mfalme atoa agizo lingine (7-14)
Wayahudi wapata kitulizo na kushangilia (15-17)</p> <p>9 Ushindi wa Wayahudi (1-19)
Sherehe ya Purimu yaanzishwa (20-32)</p> <p>10 Ukuu wa Mordekai (1-3)</p> |
|---|---|

1 Katika siku za Ahasuero,* yaani, Ahasuero aliyetawala mikoa 127^a kuanzia India mpaka Ethiopia,^Δ **2** siku hizo Mfalme Ahasuero alipokuwa akiketi kwenye kiti chake cha ufalme katika ngome ya* Shushani,^{#b} **3** katika mwaka wa tatu wa utawala wake aliwafanyia karamu wakuu na watumishi wake wote. Jeshi la Uajemi^c na Umedi,^d watu mashuhuri, na wakuu wa mikoa* walikuwa mbele yake, **4** na kwa siku nyingi, siku 180, akawaonyesha utajiri wa ufalme wake wenye utukufu, na pia ukuu, heshi-

1:1 *Inaaminiwa kwamba ni Shasta wa Kwanza, mwana wa Dario Mkuu (Dario Histaspisi). ^aAu "wilaya 127 za utawala." ^ΔAu "Kushi." 1:2 *Au "jumba la mfalme lililokuwa." 1:2, 5 [#]Au "Susa." 1:3 *Au "wilaya za utawala."

SURA YA 1

^a Est 8:9
Da 6:1

^b Ezz 4:9
Ne 1:1
Da 8:2

^c Ezz 1:2

^d Isa 21:2
Yer 51:11
Da 5:28

ma, na fahari yake. **5** Baa-da ya siku hizo kwisha, mfalme akawafanyia karamu kwa siku saba watu wote walio-kuwa katika ngome ya* Shushani,[#] wakubwa kwa wadogo, katika bustani ya jumba la mfalme. **6** Kulikuwa na vitambaa vya kitani, pamba bora, na vitambaa vya bluu vilivyofungwa kwa kamba za kitambaa laini, sufu ya zambarau iliyofungwa kwa pete za fedha, nguzo za marumaru, na makochi ya dhahabu na fedha kwenye sakafu ya mawe mekundu, lulu, na marumaru nyeupe na nyeusi.

7 Walipewa divai katika vikombe vya* dhahabu; kila kikombe kilikuwa tofauti na

1:5 *Au "jumba la mfalme la." 1:7 *Au "vyombo; bilauri za."

vikombe vingine, na divai ya kifalme ilikuwa nyingi sana, kulingana na mali ya mfalme. **8** Walikunywa kulingana na sheria ya kwamba hakuna mtu aliyelazimishwa,* kwa maana mfalme alikuwa amepanga na maofisa wa jumba la mfalme kwamba kila mtu afanye kama alivyopenda.

9 Pia, Malkia Vashti^a akawafanyia wanawake karamu katika nyumba ya kifalme ya* Mfalme Ahasuero.

10 Siku ya saba, moyo wa mfalme ulipokuwa umechangamka kwa sababu ya divai, akawaambia Mehumani, Biztha, Harbona,^b Bigtha, Abagtha, Zethari, na Karkasi, maofisa saba wa makao ya mfalme waliokuwa wahudumu wake binafsi, **11** wamlete Malkia Vashti mbele ya mfalme akiwa na taji la* malkia, ili awaonyeshe watu na wakuu urembo wake, kwa maana alikuwa mrembo sana. **12** Lakini Malkia Vashti akaendelea kukataa kuja, hakutii agizo la mfalme alilopewa na maofisa wa makao ya mfalme. Basi mfalme akakasirika sana, na ghadhabu yake ikawaka.

13 Kisha mfalme akazungumza na wanaume wenye hekima waliokuwa na ujuzi kuhusu desturi* (kwa maana hivyo ndivyo habari za mfalme ziliyoletwa kwa wale wote walioifahamu sheria na kesi za kisheria, **14** na watu walio kuwa karibu zaidi na mfalme walikuwa Karshena, Shethari, Admatha, Tarshishi, Me-

1:8 *Au "aliyezuiwa." 1:9 *Au "jumba la kifalme la." 1:11 *Au "kilemba cha." 1:13 *Au "taratibu." Tnn., "nyakati."

SURA YA 1

a Est 1:12
Est 2:1, 17

b Est 7:9

Safu ya 2

a Ezz 7:14

b Est 1:12

c Est 8:8
Da 6:8

resi, Marsena, na Memukani, wakuu saba^a wa Uajemi na Umedi, walioingia kwa mfalme na waliokuwa na vyeo vya juu zaidi katika ufalme). **15** Mfalme akauliza: "Kulingana na sheria, Malkia Vashti anapaswa kutendewaje kwa sababu hajatii agizo la Mfalme Ahasuero aliloambiwa na maofisa wa makao ya mfalme?"

16 Ndipo Memukani akajibu hivi mbele ya mfalme na wakuu: "Malkia Vashti hajamkosea mfalme peke yake,^b bali pia amewakosea wakuu wote na watu wote walio katika mikoa yote ya* Mfalme Ahasuero. **17** Kwa maana jambo alilofanya malkia litajulikana kwa wanawake wote walioolewa, nao watawadharau waume zao wakisema, 'Mfalme Ahasuero aliamuru Malkia Vashti aletwe mbele yake, lakini akakataa kuja.' **18** Leo hii mabinti wa wakuu wa Uajemi na Umedi wanaojua jambo alilofanya malkia, watawambia wakuu wote wa mfalme, na hilo litasababisha dharau na hasira nyingi. **19** Basi mfalme akipenda, na atoe amri ya kifalme itakayoandikwa katika sheria za Uajemi na Umedi, zisizoweza kubadilishwa,^c kwamba Vashti asije tena kamwe mbele ya Mfalme Ahasuero, na mfalme ampe cheo chake cha umalkia mwanamke aliye bora kuli-koyeye. **20** Na amri hiyo itakaposikiwa katika milki yake yote kubwa, wanawake wote watawaheshimu waume zao, kuanzia mkubwa mpaka mdogo zaidi."

1:16 *Au "wilaya zote za utawala za."

21 Pendekezo hilo likamfurahisha mfalme na wakuu, naye mfalme akafanya kama alivyosema Memukani. **22** Basi akatuma barua kwa mikoa yote ya ufalme,^a kila mkoa[#] kwa mwandiko wake wenyewe^Δ na kwa kila kikundi cha watu katika lugha yao wenyewe, kwamba kila mume awe bwana mkubwa[□] wa nyumba yake mwenyewe na azungumze lugha ya watu wake mwenyewe.

2 Baada ya mambo hayo, hasira kali ya Mfalme Ahasuero^b ilipopungua, akakumbuka kosa la Vashti^c na uamuzi uliofanywa kumhusu.^d **2** Ndipo wahudumu binafsi wa mfalme wakasema: “Mfalme atafutiwe wasichana warembo mabikira. **3** Na mfalme ateu wajumbe katika mikoa yote ya* milki yake^e ili wawakusanye pamoja na kuwaleta wasichana wote warembo walio mabikira kwenye nyumba ya wanawake[#] katika ngome ya^Δ Shushani.[□] Wata-tunzwa na Hegai^f towashi wa mfalme aliye mlinzi wa wanawake, nao watarembeshwa.[□] **4** Msichana atakayependwa zaidi na mfalme atakuwa malkia badala ya Vashti.”^g Na pendekezo hilo likamfurahisha mfalme, naye akafanya hivyo.

5 Kulikuwa na mwanamume fulani Myahudi aliyeishi katika ngome ya^Δ Shushani,^{□h} aliitwa Mordekaiⁱ mwana wa

1:22 *Tnn., “wilaya zote za utawala za mfalme.” #Au “wilaya ya utawala.” ^ΔAu “mtindo wake wenyewe wa kuandika.” #Au “mkuu.” 2:3 *Au “wilaya zote za utawala za.” #Au “nyumba ya harimu.” 2:3, 5, 8 ^ΔAu “jumba la mfalme la.” 2:3, 5, 8 [□]Au “Susa.” 2:3 [□]Au “watakandwa.”

SURA YA 1
a Est 3:12, 14

SURA YA 2

b Est 1:1

c Est 1:12

d Est 1:19

e Est 8:9

f Est 2:15

g Est 1:19

h Ezz 4:9
Ne 1:1
Est 1:2
Da 8:2

i Est 3:2
Est 10:3

Safu ya 2

a Mwa 49:27
1Sa 9:21

b 2Fa 24:14, 15
1Nya 3:16
2Nya 36:9, 10
Yer 22:28
Yer 24:1
Yer 37:1
Yer 52:31
Mt 1:11

c Est 2:15

d Est 2:3

e Est 2:12

f Est 3:8

g Est 2:7

h Est 4:12-14

Yairi mwana wa Shimei mwana wa Kishi, Mbenjamini,^a **6** aliyekuwa miongoni mwa watu waliopelekwa uhamishoni kutoka Yerusalemu pamoja na Mfalme Yekonia^{#b} wa Yuda, ambaye Mfalme Nebukadnega wa Babiloni alimpeleka uhamishoni. **7** Alikuwa mlezi^{*} wa Hadasa,[#] yaani, Esta binti ya ndugu ya baba yake,^c kwa maana Esta hakuwa na baba wala mama. Msichana huyo alikuwa mrembo na mwenye umbo zuri, na baba na mama yake walipokufa, Mordekai alimchukua na kumlea kama binti yake. **8** Amri na sheria ya mfalme ilipotangazwa na wasichana wengi kukusanywa kwenye ngome ya^Δ Shushani[□] chini ya utunzaji wa Hegai,^d Esta pia alipeleka kwenye nyumba ya* mfalme chini ya utunzaji wa Hegai mlinzi wa wanawake.

9 Basi msichana huyo alimpendeza Hegai na kupata upendeleo wake,^{*} basi Hegai akapanga mara moja arembeshwe^{#e} na kupewa chakula cha pekee, pia akampa wasichana saba waliochaguliwa kutoka kwa nyumba ya mfalme. Vilevile akamhamisha Esta na wale wasichana na kuwapeleka mahali bora zaidi katika nyumba hiyo ya wanawake.^Δ **10** Esta hakusema lolote kuhusu watu wake^f wala watu wake wa ukoo, kwa maana Mordekai^g alikuwa amemwagiza asimwambie yeyote.^h **11** Siku baada

2:6 *Anaitwa Yehoyakini kwenye 2Fal 24:8. 2:7 *Au “mtunzaji.” #Maana yake “Mhadasi.” 2:8 *Au “jumba la.” 2:9 *Au “upendo wake mshikamanifu.” #Au “akandwe.” ^ΔAu “katika nyumba ya harimu.”

ya siku Mordekai alikuwa akipita mbele ya ua wa nyumba ya wanawake* ili ajue hali ya Esta na mambo yaliyokuwa yakimpata.

12 Kila msichana alikuwa na zamu ya kwenda mbele ya Mfalme Ahasuero baada ya kurembeshwa kwa kipindi cha miezi 12 walichopangiwa wanawake, kwa maana huo ndio uliokuwa utaratibu wa kurembeshwa*—miezi sita kwa mafuta ya manemane^a na miezi sita kwa mafuta ya zeri^b na mafuta mbalimbali ya urembo.[#] **13** Kisha msichana angekuwa tayari kwenenda mbele ya mfalme, naye alipewa chochote alichooomba alipoondoka katika nyumba ya wanawake* kwenda kwenye nyumba ya mfalme. **14** Msichana angeingia kwa mfalme jioni, na asubuhi angerudi kwenye nyumba ya pili ya wanawake* iliyosimamiwa na Shaashgazi, towashi wa mfalme,^c mlinzi wa masuria. Hangerudi kwa mfalme tena isipokuwa iwe mfalme alipendeza naye kwa njia ya pekee na kumwita kwa jina.^d

15 Ilipofika zamu yake ya kuingia kwa mfalme, Esta binti ya Abihaili ndugu ya baba ya Mordekai, aliyemchukua na kumlea kama binti yake,^e hakuomba chochote ila vitu alivyopendekeza Hegai towashi wa mfalme, aliyekuwa mlinzi wa wanawake. (Wakati wote huo kila mtu aliyemwona Esta alipendeza naye.) **16** Esta akapelekwa kwa Mfalme Aha-

SURA YA 2

- a Met 7:17
Wim 3:6
b Mwa 43:11
1Fa 10:2
ZFa 20:13
c Est 2:3
d Est 4:11
e Est 2:7

Safu ya 2

- a Est 1:3
b Est 4:14
c Est 1:19
d Est 2:3, 4
e Est 2:5, 6
Est 3:8
f Est 2:7, 10

suro katika nyumba yake ya kifalme mwezi wa kumi, yaani, mwezi wa Tebethi* katika mwaka wa saba^a wa utawala wake. **17** Naye mfalme akampenda Esta kuliko wale wanawake wengine wote, akapata upendeleo na kibali* machoni pa mfalme kuliko wale mabikira wengine wote. Basi akamvika taji la[#] malkia na kumfanya kuwa malkia^b bada-la ya Vashti.^c **18** Naye mfalme akaandaa karamu kubwa kwa ajili ya wakuu wake wote na watumishi wake wote, karamu ya Esta. Kisha akatangaza msamaha kwa mikoa,* naye akatoa zawadi kulingana na mali ya mfalme.

19 Sasa mabikira*^d walipokusanywa mara ya pili, Mordekai alikuwa ameketi katika lango la mfalme. **20** Esta hakusema lolote kuhusu watu wake wa ukoo na watu wa taifa lake,^e kama Mordekai alivyokuwa amemwagiza; Esta aliendelea kutii maneno ya Mordekai, kama alivyofanya alipokuwa akimlea.^f

21 Siku hizo Mordekai alipokuwa akiketi katika lango la mfalme, Bighthani na Tere-shi, maofisa wawili wa makao ya mfalme, walinzi wa milango, walikasirika na kupanga njama ya kumuua Mfalme Ahasuero. **22** Lakini Mordekai akajua jambo hilo, na mara moja akamwambia Malkia Esta. Naye Esta akazungumza na mfalme kwa jina la* Mordekai. **23** Basi jambo hilo lika-

2:11, 13 *Au "nyumba ya harimu." 2:12 *Au "kukandwa." #Au "na kukandwa kwa wanawake." 2:14 *Au "nyumba ya pili ya harimu."

2:16 * Angalia Nyongeza B15. 2:17 *Au "upendo mshikamanifu." #Au "kilembe cha." 2:18 *Au "wilaya za utawala." 2:19 *Au "wasichana." 2:22 *Au "kwa niaba ya."

chunguzwa na mwishowe lika-thibitishwa, na wale wanau-me wawili wakatundikwa mti-ni; na mambo hayo yote ya-kaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati mbele ya mfalme.^a

3 Baada ya mambo hayo Mfalme Ahasuero alimpa-ndisha cheo Hamani^b mwa-na wa Hamedatha Mwangagi^c na kumkweza juu ya wakuu wengine wote katika utawa-la wake.^d **2** Watumishi wote wa mfalme waliokuwa kati-ka lango la mfalme walikuwa wakimwinamia na kumsujudia Hamani, kwa maana mfalme alikuwa ameamuru atendewe hivyo. Lakini Mordekai alika-taa kumwinamia au kumsu-judia. **3** Basi watumishi wa mfalme waliokuwa katika lan-go la mfalme wakamuuliza Mordekai: “Kwa nini unapu-za amri ya mfalme?” **4** Inga-wa siku baada ya siku wali-muuliza hivyo, hakuwasiki-liza. Kisha wakamjulisha Ha-mani ili kuona kama tabia ya Mordekai ingevumiliwa;^e kwa maana Mordekai alikuwa ame-wambia kwamba yeye ni Myahudi.^f

5 Sasa Hamani alipoona kwamba Mordekai ameka-taa kumwinamia na kumsu-ju-dia, alikasirika sana.^g **6** La-kini alichukizwa na wazo la kumuua Mordekai peke yake, kwa maana alikuwa ameambi-wa kuhusu watu wa Mordekai. Hivyo, Hamani akaanza ku-tafuta njia ya kuwaangamiza Wayahudi wote katika milki yote ya Ahasuero, watu wote wa Mordekai.

7 Katika mwezi wa kwa-nza, yaani, mwezi wa Ni-

SURA YA 2
a Est 6:1, 2

SURA YA 3

b Est 3:10
Est 8:7
Est 9:24

c Kut 17:16
Hes 24:7
Kum 25:19
1Sa 15:8, 32

d Est 1:14

e Da 6:13

f Est 2:5

g Est 5:9

Safu ya 2

a Est 1:3
Est 2:16

b Est 9:24

c Est 9:1

d Kum 4:27
Ne 1:8
Yer 50:17

e Est 1:1

f Mwa 41:42

g Est 3:1
Est 8:2

h Hes 24:7
1Sa 15:8, 32

i Est 8:9

j Da 6:8

sani,^{*} mwaka wa 12^a wa utawala wa Mfalme Ahasuero, wakapiga Puri^b (yaa-ni, Kura) mbele ya Hamani ili kuamua siku na mwezi, nayo ikaangukia mwezi wa 12, yaa-ni, Adari.^{*c} **8** Kisha Hamani akamwambia Mfalme Ahasue-ro: “Kuna watu fulani walio-tawanyika na kusambaa kati ya watu^d katika mikoa yote ya^{*} milki yako,^e ambao sheria zao ni tofauti na za watu we-n-gine wote, nao hawatii she-ria za mfalme, na wakiachwa watamletea mfalme hasara. **9** Mfalme akipenda, amri ya kuwaangamiza Wayahudi na iandikwe. Nitawapa maofisa talanta 10,000 za fedha^{*} ili waziweke katika hazina ya mfalme.”[#]

10 Ndipo mfalme akavua pete yake ya muhurif^f kuto-ka mkononi mwake, aka-mpa Hamani^g mwana wa Ha-medatha Mwangagi,^h aliyekuwa adui wa Wayahudi. **11** Mfal-me akamwambia Hamani: “Umepewa fedha na pia watu hao ili uwatendee upenda-vyo.” **12** Kisha waandishi wa mfalmeⁱ wakaitwa siku ya 13 ya mwezi wa kwanza. Wakaa-ndika^j maagizo yote ya Ha-mani kwa maliwali wa mfal-me, magavana wa mikoa,^{*} na wakuu wa vikundi mbalimbali vya watu, kila mkoa[#] kwa mwandiko wake wenyewe^Δ na kila kikundi cha watu kwa

3:7 *Angalia Nyongeza B15. 3:8 *Au “wilaya zote za utawala za.” 3:9 *Talanta ilikuwa sawa na kilogramu 34.2. Angalia Nyongeza B14. #Au labda, “Nitalipa talanta 10,000 kwenye hazina ya mfalme kwa ajili ya wale watakaofanya kazi hiyo.” 3:12 *Au “wilaya za utawala.” #Au “wilaya ya utawala.” ΔAu “mtindo wake wenyewe wa kuandika.”

luga yao wenyewe. Maagizo hayo yaliandikwa katika jina la Mfalme Ahasuero na kutiwa muhuri kwa pete ya mfalme.^a

13 Wajumbe wakapeleka kwenye mikoa yote ya* mfalme barua zilizokuwa na agizo la kuangamiza, kuua, na kuwafutilia mbali Wayahudi wote, vijana kwa wazee, wanawake kwa watoto, katika siku moja, siku ya 13 ya mwezi wa 12, yaani, mwezi wa Adari,^b na kuchukua mali zao.^c **14** Nakala ya agizo hilo ilipaswa kutolewa iwe sheria katika kila mkoa* na watu wote watangaziwe, ili wajitayarisha kwa ajili ya siku hiyo. **15** Wajumbe wakaondoka haraka^d kulingana na agizo la mfalme; sheria hiyo ilitolewa katika ngome ya* Shushani.^e Kisha mfalme na Hamani wakaketi ili kunywa, lakini kulikuwa na hali ya wasiwasi katika jiji la Shushani.^f

4 Mordekai^f alipojua mambo yote yaliyofanywa^g akararua mavazi yake, akavaa nguo za magunia na kujimwagia majivu. Kisha akaenda katikati ya jiji, akilia kwa sauti kubwa na kwa uchungu. **2** Akaenda karibu na lango la mfalme, kwa maana hakuna mtu aliyepaswa kuingia katika lango la mfalme akiwa amevaa nguo za magunia. **3** Katika kila mkoa*^h ambako neno la mfalme na amri yake ilifika, kulikuwa na maombolezo makubwa miongoni mwa Wayahudi, pia walifunga,ⁱ wakalia, na kuomboleza. Wengi wao

3:13 *Au "wilaya zote za utawala za."
3:14; 4:3 *Au "wilaya ya utawala."
3:15 *Au "jumba la mfalme la." 3:15;
4:8 *Au "Susa."

SURA YA 3

a Est 8:8
Da 6:17

b Est 9:1

c Est 8:11, 12

d Est 8:14

e Ezr 4:9
Ne 1:1
Da 8:2

SURA YA 4

f Est 2:5

g Est 3:8-11

h Est 1:1

i 2Nya 20:3
Ezr 8:21

Safu ya 2

a Da 9:3

b Est 3:9

c Est 3:8, 13

d Est 3:14, 15

e Est 2:20

f Est 2:5, 7

g Est 5:1

walilala chini katika majivu wakiwa wamevaa nguo za magunia.^a **4** Watumishi wa kike na matowashi wa Esta walipokuja na kumwambia habari hiyo, Malkia alifadhaika sana. Akaagiza Mordekai apelekwemavazi ili avae badala ya nguo za magunia, lakini Mordekai akayakataa. **5** Ndipo Esta akamwita Hathaki, mmoja wa matowashi wa mfalme, aliye-chaguliwa na mfalme kumhudumia Esta, naye akamwagiza amulize Mordekai maana ya jambo hilo na kilichokuwa ki-kiendelea.

6 Basi Hathaki akatoka na kwenda kwa Mordekai kwenye uwanja wa jiji mbele ya lango la mfalme. **7** Mordekai akamwambia yote yaliyompata na kiasi kamili cha pesa^b ambacho Hamani alikuwa ameahidi kulipa katika hazina ya mfalme ili Wayahudi waangamizwe.^c **8** Pia akampa nakala ya amri iliyoandikwa na kutolewa Shushani^d kwamba waangamizwe. Hathaki alipaswa kumwonyesha Esta na kumfanulia^e na kumwambia aende kwa mfalme kumwomba kibali na kumsihi moja kwa moja kwa niaba ya Wayahudi.

9 Basi Hathaki akarudi na kumwambia Esta mambo yote aliyosema Mordekai. **10** Kisha Esta akamwambia Hathaki amwambie hivi Mordekai:^f **11** "Watumishi wote wa mfalme na watu wa mikoa ya* mfalme wanajua kuna sheria moja tu kwa mwanamume au mwanamke yeyote atakayeingia katika ua wa ndani wa mfalme^g bila kuitwa: Mtu huyo anapaswa kuuawa; ataishi iki-

4:11 *Au "wilaya za utawala za."

wa tu mfalme atamnyooshea fimbo yake ya ufalme ya dhahabu.^a Nami sijaitwa kuingia kwa mfalme kwa siku 30 sasa.”

12 Mordekai alipopata ujumbe wa Esta, **13** akamjibu hivi Esta: “Usidhani kwa mba kwa kuwa unaishi katika makao ya mfalme unaweza kuokoka kati ya Wayahudi wengine wote. **14** Kwa maana ukikaa kimya wakati huu, Wayahudi watapata msaada na ukombozi kutoka chanzo kingine,^b lakini wewe na nyumba ya baba yako mtaangamia. Ni nani ajuaye ikiwa ume-pata cheo cha umalkia kwa ajili ya wakati kama huu?”^c

15 Kisha Esta akamjibu hivi Mordekai: **16** “Nenda, waku-sanye Wayahudi wote waliao Shushani* na mfunge^d kwa ajili yangu. Msile wala kunywa kwa siku tatu,^e usiku na mchana. Mimi pia pamoja na watumishi wangu wa kike tutafunga. Kisha nitaingia kwa mfalme, jambo ambalo ni kinyume cha sheria, na ikiwa nitaa-ngamia, acha niangamie.” **17** Basi Mordekai akaenda zake na kufanya mambo yote ambayo Esta alimwagiza afanye.

5 Siku ya tatu^f Esta akavaa mavazi yake ya kifalme na kusimama katika ua wa ndani wa nyumba ya* mfalme, sehemu iliyotazamana na nyumba ya mfalme, naye mfalme alikuwa ameketi kwenye kiti chake cha ufalme ndani ya nyumba ya mfalme akitazama langoni. **2** Mara tu mfalme alipomwona Malkia Esta akiwa amesimama kwenye ua, akafurahi

4:16 *Au “Susa.” 5:1 *Au “Jumba la.”

SURA YA 4

a Est 5:2
Est 8:4

b 1Sa 12:22
Isa 54:17

c Est 2:17

d 2Nya 20:3
Ezr 8:21

e Est 5:1

SURA YA 5

f Est 4:16

Safu ya 2

a Est 4:11
Est 8:4

b Est 3:1, 10

c Est 7:2

d Est 3:2-5

kumwona, naye mfalme akamnyooshea Esta fimbo yake ya ufalme ya dhahabu^a iliyo-kuwa mkononi mwake. Basi Esta akakaribia na kuigusa ncha ya fimbo hiyo.

3 Mfalme akamuuliza: “Malkia Esta, kuna nini? Niambie unachotaka. Hata ukiomba nusu ya ufalme wangu utape-wa!” **4** Esta akajibu: “Mfalme akipenda na aje leo pamoja na Hamani^b kwenye karamu ambayo nime mwandalia.” **5** Basi Mfalme akawaambia watumishi wake: “Mwambieni Hamani aje haraka, kama Esta anavyoomba.” Basi, mfalme na Hamani wakaenda kwenye karamu ambayo Esta alikuwa ameandaa.

6 Karamu ya divai ilipokuwa ikiendelea, mfalme akamwambia Esta: “Una ombi gani? Utapewa utakachoomba! Na unataka nini? Hata ukiomba nusu ya ufalme wangu, utapewa!”^c **7** Esta akamjibu: “Hili ndilo ombi langu na jambo ninalotaka, **8** Ikiwa nimepata kibali chako Ee mfalme, nawe mfalme ukipe-nda kutimiza ombi langu na kunipa ninachotaka, naomba mfalme uje pamoja na Hamani kwenye karamu ambayo nitawaandalia kesho; na kesho nitafanya kama unavyosema mfalme.”

9 Siku hiyo Hamani aliondoka akiwa na shangwe na uchangamfu moyoni. Lakini Hamani alipomwona Mordekai katika lango la mfalme na kutambua kwamba haku-simama wala kutetemeka alipomwona, Hamani alimkasirikia sana Mordekai.^d **10** Hata hivyo, Hamani akajizua na

kwenda nyumbani kwake. Kisha akawatuma watu wawaite marafiki zake na pia Zereshi^a mke wake. **11** Hamani aka-jigamba kuhusu utajiri wake mwingi, wanawe wengi,^b na jinsi mfalme alivyompandisha cheo na kumkweza juu ya wakuu na watumishi wa mfalme.^c

12 Hamani akaendelea kusema: "Isitoshe, Malkia Esta hakumwalika mtu mwingine yeyote isipokuwa mimi nimsidikize mfalme kwenye karamu aliyoandaa.^d Kesho pia amenialika mimi ili niwe naye pamoja na mfalme.^e **13** Lakin mambo hayo yote hayaniridhishi ninapoendelea kumwona Mordekai Myahudi akiwa ameketi kwenye lango la mfalme." **14** Ndipo Zereshi mke wake na marafiki zake wote wakamwambia: "Agiza mti we-nye kimo cha mikono 50* usimamishwe. Kisha asubuhi umwambie mfalme kwamba Mordekai anapaswa kutundikwa juu yake.^f Halafu uende na mfalme kujifurahisha kwenye karamu." Pendekezo hilo likampendeza Hamani, kwa hiyo akaagiza mti huo usimamishwe.

6 Usiku huo mfalme hakupata usingizi.* Hivyo, akaagiza kitabu cha historia ya nyakati kiletwe,^g nacho kikasoma mbele yake. **2** Wakapata kwamba kilikuwa kimeandikwa habari ambazo Mordekai alitoa kuhusu Bighthana na Tereshi, wale maofisa wawili wa makao ya mfalme, walinzi wa milango, waliopanga njama ya kumuua Mfalme Aha-

5:14 *Karibu mita 22.3 (futi 73). Angalia Nyongeza B14. 6:1 *Tnn., "usingizi wa mfalme ulitoweka."

SURA YA 5

a Est 5:14
Est 6:13

b Est 9:7-10

c Est 3:1

d Est 5:5

e Est 5:8

f Est 6:4
Est 7:9

SURA YA 6

g Est 10:2

Safu ya 2

a Est 2:21, 23

b Est 4:11

c Est 5:14

d Est 3:1

e Est 3:2
Est 5:11

f Est 8:15

g Mwa 41:42, 43

sueru.^a **3** Mfalme akauliza: "Mordekai amepewa heshima na shukrani gani kwa tendo hilo?" Ndipo watumishi binafisi wa mfalme wakasema: "Hajafanyiwa jambo lolote."

4 Baadaye mfalme akauliza: "Ni nani aliye katika ua?" Basi Hamani alikuwa amekuja katika ua wa nje^b wa nyumba ya* mfalme ili azungumze na mfalme kuhusu kumtundika Mordekai juu ya mti aliokuwa ameutengeneza kwa ajili yake.^c **5** Watumishi wa mfalme wakamjibu: "Ni Hamani^d aliyesimama kwenye ua." Mfalme akasema: "Mwambieni aingie."

6 Hamani alipoingia, mfalme akamwambia: "Afanyiwe nini mtu ambaye mfalme angependa kumheshimu?" Hamani akajiambia moyoni: "Mfalme angependa kumheshimu nani isipokuwa mimi?"^e **7** Basi Hamani akamwambia mfalme: "Mtu ambaye mfalme angependa kumheshimu, **8** na aletewe mavazi ya kifalme^f ambayo mfalme huvaa na farasi ambaye humbeba mfalme, farasi mwenye taji la kifalme kichwani. **9** Kisha mmoja wa wakuu wa cheo cha juu wa mfalme ape-we hayo mavazi na yule farasi, nao wanapaswa kumvisha mtu ambaye mfalme angependa kumheshimu, na wamtembeze katika uwanja wa jiji akiwa juu ya farasi. Kisha wanapaswa kutangaza kwa sauti mbele yake: 'Hivi ndivyo anavyofanyiwa mtu ambaye mfalme angependa kumheshimu!'"^g **10** Mara moja mfalme akamwambia Hamani: "Fanya

6:4 *Au "jumba la."

haraka! Chukua mavazi na farasi, nawe umfanyie Mordekai kama ulivyosema, yule Myahudi anayeketi katika lango la mfalme. Usikose kumfanyia lolote kati ya mambo uliyosema.”

11 Basi Hamani akachukua mavazi hayo na farasi, akamvisha Mordekai^a na kumtembeza katika uwanja wa jiji akiwa juu ya farasi na kutangaza kwa sauti mbele yake: “Hivi ndivyo anavyofanyiwa mtu ambaye mfalme angependa kumheshimu!” **12** Baadaye Mordekai akarudi kwenye lango la mfalme, lakini Hamani akaenda haraka nyumbani kwake, akiomboleza akiwa amefunika kichwa chake. **13** Hamani alipomsimulia Zereshi mke wake^b na marafiki zake wote mambo yaliyompata, watu wake wenye hekima na Zereshi mke wake wakamwambia: “Ikiwa Mordekai ambaye umeanza kuanguka mbele yake ni wa uzao wa Kiyahudi,* hutaweza kumshinda; kwa hakika utaanguka mbele yake.”

14 Walipokuwa wakizungumza naye, maofisa wa makao ya mfalme wakaja na kumchukua Hamani na kumpeleka haraka kwenye karamu ambayo Esta alikuwa ameandaa.^c

7 Basi mfalme na Hamani^d wakaja kwenye karamu ya Malkia Esta. **2** Mfalme akamuuliza tena Esta siku ya pili wakati wa karamu ya divai: “Malkia Esta, una ombi gani? Utapewa unachoomba. Unataka nini? Hata ukiomba nusu ya ufalme wangu utapewa!”^e

6:13 *Tnn., “anatokana na mbegu ya Wayahudi.”

SURA YA 6

a Est 2:5, 6

b Est 5:10, 14

c Est 5:8

SURA YA 7

d Est 3:1

e Est 5:3, 6

Safu ya 2

a Est 2:5, 7

b Est 3:8, 9

c Est 3:13
Est 4:7, 8

d Est 1:10

3 Malkia Esta akajibu: “Ikiwa nimepata kibali chako, Ee mfalme, nawe mfalme ukipe nda, naomba uuokoe uhai wangu,* na pia uhai wa watu wangu.^a **4** Kwa maana tumeuzwa,^b mimi na watu wangu, tuangamizwe, tuuawe, na kufutiliwa mbali.^c Kama tungeuzwa tuwe watumwa wa kiume na wa kike, ningekaa kimya. Lakini msiba huu haufai, kwa sababu utamletea mfalme hasara.”

5 Ndipo mfalme Ahasuero akamuuliza Malkia Esta: “Ni nani huyo, na yuko wapi mwanamume aliyethubutu kufanya jambo hilo?” **6** Esta akasema: “Mpinzani na adui ni huyu Hamani mwovu.”

Hamani akaogopa sana kwa sababu ya mfalme na malkia. **7** Mfalme akasimama kwa hasira na kutoka kwenye karamu ya divai, akaenda kwenye bustani ya jumba la mfalme, lakini Hamani akasimama ili kumsihi Malkia Esta auokoe uhai wake,* kwa maana alijua mfalme alikuwa amezimia kumwadhibu. **8** Mfalme aliporudi kutoka kwenye bustani ya jumba la mfalme na kuingia katika nyumba ya karamu ya divai, alimwona Hamani akiwa amejiangusha kwenye kochi, mahali alipokuwa Esta. Mfalme akasema: “Je, sasa anataka kumbaka malkia katika nyumba yangu mwenyewe?” Mara tu maneno hayo yalipotoka kinywani mwa mfalme, wakaufunika uso wa Hamani. **9** Harbana,^d mmoja wa maofisa wa makao ya mfalme akasema: “Pia

7:3 *Au “nafsi yangu.” 7:7 *Au “nafsi yake.”

Hamani alitengeneza mti kwa ajili ya Mordekai^a aliyetoa habari iliyomwoko mfalme.^b Mti huo wenye kimo cha mikono 50* umesimamishwa nyumbani kwa Hamani." Ndipo mfalme akasema: "Mtundikeni juu yake." **10** Basi wakamtundika Hamani kwenye mti aliokuwa ameutengeneza ili kumtundika Mordekai juu yake, na nasira ya mfalme ikatulua.

8 Siku hiyo Mfalme Ahasuero akampa Malkia Esta nyumba* ya Hamani^c aliyekuwa adui ya Wayahudi;^d naye Mordekai akaja mbele ya mfalme, kwa maana Esta alikuwa amemfunulia kuhusu uhushiano wao wa kifamilia.^e **2** Kisha mfalme akavua pete yake ya muhuri^f aliyokuwa amepokonya Hamani, akampa Mordekai. Naye Esta akamweka Mordekai kuwa msimamizi wa nyumba ya Hamani.^g

3 Zaidi ya hayo, Esta akazungumza tena na mfalme. Akaanguka chini miguuni pake, akalia na kumsihi mfalme akomeshe madhara ya Hamani Mwangagi na njama aliyopanga dhidi ya Wayahudi.^h **4** Mfalme akamnyooshea Esta fimbo ya ufalme ya dhahabu,ⁱ naye Esta akainuka na kusimama mbele ya mfalme. **5** Esta akasema: "Ukipe nda Ee mfalme na ikiwa nimepata kibali chako, na ikiwa ni jambo jema kwako mfalme, nawe umependezwa nami, acha agizo liandikwe la kufuta barua za njama ya Hamani/mwana wa Hamedatha Mwangagi,^k alizoandika ili kuwaangamiza Wayahudi katika mi-

7:9 *Karibu mita 22.3 (futi 73). Angalia Nyongeza B14. 8:1 *Au "mali yote."

SURA YA 7

a Est 5:14

b Est 6:2

SURA YA 8

c Est 5:11

d Est 3:8
Est 9:24

e Est 2:5, 7

f Mwa 41:41, 42
Est 3:10
Da 6:17

g Da 2:48

h Est 3:9
Est 7:4
Est 9:24, 25

i Est 4:11

j Est 3:12, 14

k Kut 17:16
Hes 24:7
Kum 25:19
1Sa 15:8, 33

Safu ya 2

a Est 8:1

b Est 7:10

c Da 6:8, 15

d Da 6:1

e Est 9:3

f Est 8:2

koa yote ya* mfalme. **6** Kwa maana ninawezaje kuvumilia kuona msiba utakaowapata watu wangu, na ninawezaje kuvumilia kuona watu wangu wa ukoo wakiangamizwa?"

7 Basi Mfalme Ahasuero akamwambia Malkia Esta na Mordekai Myahudi: "Tazama! Nimempa Esta nyumba ya Hamani,^a naye Hamani ametundikwa mtini,^b kwa sababu alipanga njama ya kuwashambulia* Wayahudi. **8** Sasa andikeni katika jina la mfalme jambo lolote mnaloona linafaa kwa niaba ya Wayahudi nanyi mlitie muhuri kwa pete ya mfalme, kwa maana agizo lililoandikwa katika jina la mfalme na kutiwa muhuri kwa pete ya mfalme haliwezi kufutwa."^c

9 Ndipo waandishi wa mfalme wakitwa wakati huo katika mwezi wa tatu, yaani, mwezi wa Sivani,* siku ya 23, wakaandika mambo yote ambayo Mordekai aliwaamuru Wayahudi, na pia maliwali,^d magavana, na wakuu wa mikoa^{ae} kuanzia India mpaka Ethiopia, mikoa^a 127, kila mkoa^Δ kwa mwandiko wake wenyewe[®] na kila kikundi cha watu kwa lugha yao wenyewe na kwa Wayahudi katika mwandiko wao wenyewe[□] na lugha yao.

10 Aliandika agizo hilo katika jina la Mfalme Ahasuero na kulitia muhuri kwa pete ya mfalme,^f kisha akatu-

8:5 *Au "wilaya zote za utawala za." 8:7 *Tnn., "aliunyoosha mkono wake kwa nguvu dhidi ya." 8:9 *Angalia Nyongeza B15. ^aAu "wilaya za utawala." ^ΔAu "wilaya ya utawala." [®]Au "mtindo wake wenyewe wa kuandika." [□]Au "mtindo wao wenyewe wa kuandika."

ma barua za agizo hilo kupitia wajumbe walioendesha farasi; farasi hao wenye mbio walitumiwa kusafirisha barua, nao walizalishwa kwa ajili ya utumishi wa mfalme. **11** Katika barua hizo mfalme aliwaruhusu Wayahudi katika majiji yote wakusanyike ili walinde uhai wao* na kuangamiza, kuuu, na kuharibu jeshi lolote la taifa lolote au mkoa[#] ambao huenda ungewashambulia wao, kutia ndani wanawake na watoto wao, na kuchukua mali zao.^a **12** Wangefanya hivyo siku ileile katika mikoa yote ya* Mfalme Ahasuero, siku ya 13 ya mwezi wa 12, yaani, mwezi wa Adari.^{#b} **13** Maandishi* ya agizo hilo yalipaswa kutangazwa kuwa sheria katika mikoa yote.[#] Watu wote walipaswa kutangaziwa agizo hilo, ili Wayahudi wajitayarisha siku hiyo kulipiza kisasi dhidi ya maadui wao.^c **14** Wajumbe walioendesha farasi wa kusafirisha barua waliotumiwa katika utumishi wa mfalme wakaondoka haraka na kwa kasi kulingana na agizo la mfalme. Sheria hiyo ilitangazwa pia katika ngome ya* Shushani.^{#d}

15 Naye Mordekai akatoka mbele ya mfalme akiwa amevaa mavazi ya kifalme ya rangi ya bluu na nyeupe, taji kubwa la dhahabu, na joho la kitambaa bora cha sufya za zambarau.^e Na jiji la Shushani[#] likapiga kelele kwa sha-

8:11 *Au "nafsi zao." #Au "wilaya ya utawala." 8:12; 9:2 *Au "wilaya zote za utawala za." 8:12; 9:1 #Angalia Nyongeza B15. 8:13 *Au "Nakala." 8:13, 17; 9:4 #Au "wilaya zote za utawala." 8:14 *Au "jumba la mfalme la." 8:14, 15 #Au "Susa."

SURA YA 8

a Est 9:5-10

b Est 3:13
Est 9:1, 2
Est 9:16, 17

c Zb 149:6, 7

d Ezr 4:9
Ne 1:1
Est 1:2
Da 8:2

e Est 6:7, 8

Safu ya 2

a Zek 8:23

SURA YA 9

b Est 3:7
Est 8:11, 12

c Est 3:13

d Kum 32:36
2Sa 22:41

e Est 1:1

f Est 8:17

g Da 6:1

h Est 8:15

ngwe. **16** Wayahudi wakapata kitulizo,* wakafurahi, wakashangilia, na kupata heshima. **17** Na katika mikoa yote[#] na majiji yote, popote ambapo agizo la mfalme na sheria yake ilifika, Wayahudi walifurahi na kushangilia, wakafanya karamu na kushe-rehekea. Watu wengi wa mataifa yaliyokuwa nchini walikuwa wakijitangaza kuwa Wayahudi,^a kwa maana waliwagopa Wayahudi.

9 Siku ya 13 ya mwezi wa 12, yaani, mwezi wa Adari,^{#b} wakati ambapo agizo na sheria ya mfalme ilipaswa kutekelezwa,^c siku ambayo maadui wa Wayahudi walitarajia kuwashinda, mambo yaligeuka, Wayahudi wakawashinda wote waliowachukia.^d **2** Wayahudi wakakusanyika pamoja katika majiji yao kwenye mikoa yote ya* Mfalme Ahasuero^e ili kuwashambulia wale waliotaka kuwadhuru, na haku-na mtu aliyeweza kuwazuia, kwa sababu mataifa yote yaliwaogopa sana.^f **3** Na wakuu wote wa mikoa,^{*} maliwali,^g magavana, na watu waliofanya kazi za mfalme waliwau-nga mkono Wayahudi, kwa sababu walimwogopa Mordekai. **4** Sasa Mordekai alikuwa na mamlaka^h katika nyumba ya* mfalme, na umaarufu wake ulikuwa ukienea kotekote katika mikoa yote,[#] kwa sababu mamlaka ya Mordekai yalizidi kuongezeka.

5 Wayahudi waliwashambulia kwa upanga maadui wao wote, wakawaua na

8:16 *Tnn., "wakaona nuru." 9:3 *Au "wilaya za utawala." 9:4 *Au "jumba la."

kuwaangamiza; waliwatendea walivyotaka wale walio-wachukia.^a **6** Katika ngome ya* Shushani,^{#b} Wayahudi waliwaua na kuwaangamiza wanaume 500. **7** Pia, waliwaua Parshandatha, Dalfo-ni, Aspatha, **8** Poratha, Adalia, Aridatha, **9** Parmashta, Arisai, Aridai, na Vaizatha, **10** wana kumi wa Hamani mwana wa Hamedatha, adui ya Wayahudi.^c Lakini baada ya kuwaua, hawakuwepora chochote.^d

11 Siku hiyo, mfalme alijulishwa idadi ya watu waliouawa katika ngome ya* Shushani.[#]

12 Mfalme akamwambia Malkia Esta: "Katika ngome ya* Shushani[#] Wayahudi wamewaua watu 500 na pia wana kumi wa Hamani. Unafikiri wamewaua watu wangapi katika mikoa mingine ya[^] mfalme?^e Sasa una ombi gani? Utapewa unachotaka. Unataka nini kingine? Kitatimizwa."

13 Esta akajibu: "Ukipenda Ee mfalme,^f Wayahudi walio Shushani[#] waruhusiwe kesho pia kutekeleza sheria ya leo;^g agiza wana kumi wa Hamani watundikwe mtini."^h **14** Basi mfalme akaagiza jambo hilo lifanywe. Sheria ikatangazwa Shushani,[#] na wana kumi wa Hamani wakatundikwa.

15 Wayahudi waliokuwa Shushani[#] wakakusanyika pamoja tena siku ya 14 ya mwezi wa Adariⁱ na kuwaua watu 300 huko Shushani,[#] lakini hawakuwepora chochote.

9:6, 11, 12 *Au "jumba la mfalme la." 9:6, 11-15, 18 *Au "Susa." 9:12 [^]Au "wilaya nyingine za utawala za."

SURA YA 9

a Est 8:11
b Ezz 4:9
Ne 1:1
Est 1:2
Da 8:2
c Est 3:8, 10
Est 7:4-6
d Est 8:11
Est 9:16
e Est 9:16
f Est 5:8
Est 7:3
Est 8:5
g Est 8:11
h Est 7:10
i Est 9:21, 22

Safu ya 2

a Est 7:3
b Est 8:13
Zb 149:6, 7
c Est 9:1, 2
d Est 9:13, 15
e Zb 124:2, 6
f Ne 8:10
g Est 2:5, 6
h Est 4:1-3

16 Wayahudi wengine wote waliokuwa katika mikoa ya* mfalme, wakakusanyika pamoja pia ili kulinda uhai wao.^{#a} Wakawaangamiza maadui wao,^b wakawaua watu 75,000 kati ya wale waliowachukia; lakini hawakuwepora chochote. **17** Mambo hayo yalitukia siku ya 13 ya mwezi wa Adari, wakapumzika siku ya 14 ya mwezi huo na kuifanya kuwa siku ya karamu na kushangilia.

18 Wayahudi waliokuwa Shushani[#] wakakusanyika pamoja siku ya 13^c na ya 14,^d wakapumzika siku ya 15 na kuifanya kuwa siku ya karamu na kushangilia. **19** Ndiyo sababu Wayahudi wa mashambani walioishi katika majiji ya wilaya zilizo mbali waliifanya siku ya 14 ya mwezi wa Adari iwe siku ya karamu na kushangilia, siku ya kusherehekea,^e na siku ya kupeana mafungu ya vyakula.^f

20 Mordekai^g akaandika matukio hayo kisha akatuma barua rasmi kwa Wayahudi wote waliokuwa katika mikoa yote ya* karibu na ya mbali ya Mfalme Ahasuero. **21** Akawaagiza waadhimisha siku ya 14 ya mwezi wa Adari, na pia siku ya 15, kila mwaka, **22** kwa sababu katika siku hizo Wayahudi walipumzika kutokana na usumbufu wa maadui wao, na mwezi huo huzuni yao ikageuzwa kuwa shangwe, na maombolezo yao^h kuwa siku ya kusherehekea. Walipaswa kuadhimisha siku hizo zikiwa siku za karamu na

9:16 *Au "wilaya za utawala za." #Au "kutetea nafsi zao." 9:20 *Au "wilaya zote za utawala za."

kushangilia, za kupeana mafungu ya vyakula, na za kuwapa maskini zawadi.

23 Na Wayahudi wakakubali kuendelea kufanya sherehe waliyoanzisha na kufanya mambo waliyoandikiwa na Mordekai. **24** Kwa maana Hamani^a mwana wa Hamedatha Mwangagi,^b adui ya Wayahudi wote, alikuwa amepanga njama ya kuwaangamiza Wayahudi,^c na alikuwa amepiga Puri,^d yaani, Kura, ili kuwatisha na kuwaangamiza. **25** Lakini Esta alipokuja mbele ya mfalme, mfalme alitoa agizo lili-loandikwa hivi:^e “Njama yake mbaya dhidi ya Wayahudi^f na irudi juu ya kichwa chake mwenyewe”; nao wakamtuandika yeye pamoja na wanawe mtini.^g **26** Ndiyo sababu waliiziita siku hizo Purimu, kutokana na jina la ile Puri.^{*h} Kwa hiyo, kwa sababu ya mambo yote yaliyoandikwa katika barua hiyo na yale waliyoona kuhusiana na tukio hilo na mambo yaliyowapata, **27** Wayahudi pamoja na wazao wao na wote waliojiunga nao wakajitwika wajibu waⁱ kusherehekea siku hizo mbili bila kukosa na kutekeleza mambo yote yaliyoandikwa kuhusu siku hizo, wakati uliowekwa kila mwaka. **28** Siku hizo zilipaswa kukumbukwa na kuadhimishwa na kila kizazi, katika kila familia, kila mkoa,^{*} na kila jiji; na Wayahudi hawakupaswa kuacha kuzikumbuka siku hizo za Pu-

9:26 *Neno “Puri,” linamaanisha “Kura.” Neno hilo katika wingi ni “Purimu,” nalo lilianza kutumiwa kurejelea sherehe ya Wayahudi inayosherehekewa mwezi wa 12 wa kalenda takatifu. Angalia Nyongeza B15. **9:28** *Au “wilaya ya utawala.”

SURA YA 9

a Est 3:1

b Kut 17:16
Hes 24:7
Kum 25:19
1Sa 15:8, 33

c Est 3:8, 9

d Est 3:7

e Est 8:10

f Est 8:3

g Est 5:14
Est 7:10
Est 9:14

h Est 3:7

i Law 24:22
Est 8:17

Safu ya 2

a Est 8:9

b Est 1:1

c Est 9:20, 21

d Est 9:27

e 2Nya 20:3

f Est 4:1

g Est 9:26

SURA YA 10

h Est 2:5, 6

i Est 8:15
Da 2:48j Ezr 4:15
Est 6:1k Est 1:3
Da 6:15

rimu wala wazao wao kuacha kuziadhimisha.

29 Kisha Malkia Esta, binti ya Abihaili, na Mordekai Myahudi wakaandika kwa mamla-ka kamili ili kuthibitisha barua ya pili kuhusu Purimu. **30** Mordekai akawatumia barua rasmi Wayahudi wote waliokuwa katika mikoa 127^a ya* milki ya Ahasuero,^b kwa maneno ya amani na kweli **31** ili kuthibitisha kuadhimishwa kwa siku za Purimu katika nyakati zilizowekwa, kama walivyoagizwa na Mordekai Myahudi na Malkia Esta^c na kama walivyojitwika wajibu, wao na wazao wao,^d pamoja na kufunga^e na kutoa dua.^f **32** Na amri ya Esta ilitibitishwa mambo hayo kuhusu Purimu,^g nayo ikaandikwa katika kitabu.

10 Mfalme Ahasuero akaa-muru watu wafanye kazi ya kulazimishwa katika nchi na katika visiwa vya bahari.

2 Na matendo yake yote makuu na yenye nguvu, na pia habari kamili kuhusu ukuu wa Mordekai^h ambao mfalme alimpa alipomkweza,ⁱ je, haya-jaandikwa katika kitabu cha historia ya nyakati^j za wafalme wa Umedi na Uajemi?^k

3 Kwa maana Mordekai Myahudi ndiye aliyekuwa wa pili kwa cheo kutoka kwa Mfalme Ahasuero. Alikuwa mkuu* miongoni mwa Wayahudi na aliheshimiwa na ndugu zake kwa ujumla,[#] naye aliyasaidia watu wake na kutetea masilahi ya[^] wazao wao wote.

9:30 *Au “wilaya 127 za utawala za.” **10:3** *Au “Alithamaniwa sana.” [#]Tnn., “umati wa ndugu zake.” [^]Tnn., “kuzungumza kuhusu amani kwa niaba ya.”

AYUBU

YALIYOMO

- 1 Utimilifu wa Ayubu na mali zake (1-5)
Shetani atilia shaka nia ya Ayubu (6-12)
Ayubu apoteza mali na watoto wake (13-19)
Ayubu hamlaumu Mungu (20-22)
- 2 Shetani atilia shaka tena nia ya Ayubu (1-5)
Shetani aruhusiwa kugusa mwili wa Ayubu (6-8)
Mke wa Ayubu: "Mtukane Mungu, ufe!" (9, 10)
Ayubu atembelewa na marafiki watatu (11-13)
- 3 Ayubu ajuta kuzaliwa (1-26)
Auliza kwa nini anateseka (20, 21)
- 4 Elifazi azungumza kwa mara ya kwanza (1-21)
Adhihakiti utimilifu wa Ayubu (7, 8)
Asimulia ujumbe kutoka kwa kiumbe wa roho (12-17)
'Mungu hana imani na watumishi wake' (18)
- 5 Elifazi aendelea kuzungumza (1-27)
'Mungu huwanasa wenye hekima katika ujanja wao' (13)
'Ayubu hapaswi kukataa nidhamu ya Mungu' (17)
- 6 Jibu la Ayubu (1-30)
Adai kwamba ana sababu ya kulia (2-6)
Wafariji wake ni wenye hila (15-18)
'Maneno ya unyoofu hayaumizi!' (25)
- 7 Ayubu aendelea kujibu (1-21)
Maisha ni kama kazi ya kulazimishwa (1, 2)
'Kwa nini umenifanya niwe shabaha yako?' (20)
- 8 Bildadi azungumza kwa mara ya kwanza (1-22)
Adai kwamba watoto wa Ayubu wametenda dhambi (4)
'Ikiwa ungekuwa safi, Mungu angekulinda' (6)
Adai kwamba Ayubu amemkataa Mungu (13)
- 9 Jibu la Ayubu (1-35)
Mwanadamu anayeweza kufa hawezi kushindana na Mungu (2-4)
'Mungu hufanya mambo yasiyochunguzika' (10)
Mtu hawezi kubishana na Mungu (32)
- 10 Ayubu aendelea kujibu (1-22)
'Kwa nini Mungu anapambana nami?' (2)
Mungu si kama Ayubu anayeweza kufa (4-12)
'Naomba nipate kitulizo kidogo' (20)
- 11 Sofari azungumza kwa mara ya kwanza (1-20)
Amshutumu Ayubu kwa sababu ya maneno yake yasiyo na maana (2, 3)
Amwambia Ayubu aache uovu (14)
- 12 Jibu la Ayubu (1-25)
'Mimi si duni kwenu' (3)
'Nimekuwa kichekesho' (4)
'Mungu ana hekima' (13)
Mungu ni mkuu kuliko waamuzi na wafalme (17, 18)
- 13 Ayubu aendelea kujibu (1-28)
'Ni afadhali nizungumze na Mungu' (3)
'Ninyi ni matabibu wasiofaa kitu' (4)
'Najua sina kosa' (18)
Auliza kwa nini Mungu anamwona kuwa adui (24)
- 14 Ayubu aendelea kujibu (1-22)
Maisha ya mwanadamu ni mafupi na yamejaa taabu (1)
'Hata mti una tumaini' (7)
'Laiti ungenificha Kaburini!' (13)
'Mtu akifa, je, anaweza kuishi tena?' (14)
Mungu ataitamani sana kazi ya mikono yake (15)
- 15 Elifazi azungumza kwa mara ya pili (1-35)
Adai kwamba Ayubu hamwogopi Mungu (4)
Asema Ayubu ana kimbelembele (7-9)
'Mungu hawaamini watakatifu wake' (15)
'Anayeteseka ni mwovu' (20-24)

- 16 Jibu la Ayubu (1-22)
'Ninyi ni wafariji wasumbufu!' (2)
Adai kwamba Mungu anamfanya kuwa shabaha yake (12)
- 17 Ayubu aendelea kujibu (1-16)
"Wadhihakii wananzunguka" (2)
"Amenifanya niwe kitu cha kudharauliwa" (6)
"Kaburi litakuwa makao yangu" (13)
- 18 Bildadi azungumza kwa mara ya pili (1-21)
Aeleza yatakayowapata waovu (5-20)
Adai Ayubu hamjui Mungu (21)
- 19 Jibu la Ayubu (1-29)
Akataa kukemewa na "rafiki" zake (1-6)
Asema kwamba ameachwa (13-19)
"Mkombozi wangu yuko hai" (25)
- 20 Sofari azungumza kwa mara ya pili (1-29)
Adai kwamba Ayubu amemtukana (2, 3)
Adai kwamba Ayubu ni mwovu (5)
Adai kwamba Ayubu anafurahia dhambi (12, 13)
- 21 Ayubu ajibu (1-34)
'Kwa nini waovu wanafanikiwa?' (7-13)
Afichua hila za "wafariji" wake (27-34)
- 22 Elifazi azungumza kwa mara ya tatu (1-30)
'Mwanadamu ana faida gani kwa Mungu?' (2, 3)
Adai kwamba Ayubu ni mwenye pupa na hatendi haki (9)
'Mrudie Mungu, utaridishiwa hali njema' (23)
- 23 Ayubu ajibu (1-17)
Ataka kupeleka kesi yake mbele za Mungu (1-7)
Asema kwamba hampati Mungu (8, 9)
"Nimefuata njia yake bila kukengeuka" (11)
- 24 Ayubu aendelea kujibu (1-25)
'Kwa nini Mungu haweki wakati wa hukumu?' (1)
Asema kwamba Mungu ameruhusu uovu (12)
Watenda dhambi wanapenda giza (13-17)
- 25 Bildadi azungumza kwa mara ya tatu (1-6)
- 'Mwanadamu anawezaje kuwa bila hatia mbele za Mungu?' (4)
Adai kwamba utimilifu wa mwanadamu ni wa bure (5, 6)
- 26 Ayubu ajibu (1-14)
"Jinsi mliyomsaidia mtu asiye na uwezo!" (1-4)
'Mungu anaining'iniza dunia mahali pasipo na kitu' (7)
'Ni kingo tu za njia za Mungu' (14)
- 27 Ayubu aazimia kuendelea kuwa mtimilifu (1-23)
"Sitaukana utimilifu wangu" (5)
Anayemkataa Mungu hana tumaini (8)
"Kwa nini mazungumzo yenu hayana maana yoyote?" (12)
Mtu mwovu habaki na chochote (13-23)
- 28 Ayubu aonyesha tofauti iliyopo kati ya hazina za dunia na hekima (1-28)
Jitihada za wanadamu za kuchimba madini (1-11)
Hekima ina thamani kuliko lulu (18)
Kumwogopa Yehova ndiyo hekima ya kweli (28)
- 29 Ayubu akumbuka maisha mazuri aliyokuwa nayo kabla ya mateso (1-25)
Aliheshimiwa kwenye lango la jiji (7-10)
Jinsi alivyokuwa akitenda haki awali (11-17)
Kila mtu alisikiliza ushauri wake (21-23)
- 30 Ayubu aeleza jinsi maisha yake yalivyobadilika (1-31)
Adhihakiwa na watu wasiofaa kitu (1-15)
Yaonekana ni kama Mungu hamsaidii (20, 21)
"Ngozi yangu imekuwa nyeusi" (30)
- 31 Ayubu atetea utimilifu wake (1-40)
"Agano na macho yangu" (1)
Aomba Mungu ampime (6)
Hakuwa mzini (9-12)
Hakupenda pesa (24, 25)
Hakuabudu sanamu (26-28)
- 32 Kijana Elihu ajiunga na mazungumzo (1-22)
Amkasirikia Ayubu na rafiki zake (2, 3)
Alisubiri kwa heshima kabla ya kuzungumza (6, 7)

- Umri peke yake haumfanyi mtu awe na hekima (9)
Elihu atamani kuongea (18-20)
- 33 Elihu amkaripia Ayubu kwa sababu ya kujiona kuwa mwadilifu (1-33)
Fidia yapatikana (24)
Kurudia nguvu za ujana (25)
- 34 Elihu atetea haki ya Mungu na njia zake (1-37)
Ayubu asema kwamba Mungu alimnyima haki (5)
Mungu wa kweli hawezi kamwe kutenda uovu (10)
Ayubu hana ujuzi (35)
- 35 Elihu ataja mawazo yasiyofaa ya Ayubu (1-16)
Ayubu asema yeye ni mwadilifu kuliko Mungu (2)
Mungu yuko juu sana, haathiriwi na dhambi (5, 6)
Ayubu anapaswa kumngojea Mungu (14)
- 36 Elihu autukuza ukuu wa Mungu usiochunguzika (1-33)
Wanaotii wanafanikiwa; wanaomkataa Mungu wanakataliwa (11-13)
‘Ni nani aliye mfundishaji kama Mungu?’ (22)
Ayubu anapaswa kumtukuza Mungu (24)
“Mungu ni mkuu kuliko tunavyoweza kujua” (26)
Mungu hudhibiti mvua na radi (27-33)
- 37 Nguvu za asili zinafunua ukuu wa Mungu (1-24)
- Mungu anaweza kusimamisha shughuli za wanadamu (7)
‘Tafakari kazi za Mungu zinazostaajabisha’ (14)
Wanadamu hawawezi kumwelewa Mungu (23)
Hakuna mwanadamu anayepaswa kukifikiri kwamba ana hekima (24)
- 38 Yehova afundisha kuhusu udogo wa mwanadamu (1-41)
‘Ulikuwa wapi nilipoiumba dunia?’ (4-6)
Wana wa Mungu walishangilia kwa sauti (7)
Maswali kuhusu matukio ya asili (8-32)
“Sheria zinazoongoza mbingu” (33)
- 39 Uumbaji wa wanyama waonyesha ujinga wa mwanadamu (1-30)
Mbuzi wa milimani na paa (1-4)
Punda mwitu (5-8)
Fahali mwitu (9-12)
Mbuni (13-18)
Farasi (19-25)
Kipanga na tai (26-30)
- 40 Yehova amuuliza maswali zaidi (1-24)
Ayubu akiri hana la kusema (3-5)
“Je, utatilia shaka haki yangu?” (8)
Mungu aeleza kuhusu nguvu za Behemothi (15-24)
- 41 Mungu aeleza kuhusu Lewiathani anayestaajabisha (1-34)
- 42 Ayubu amjibu Yehova (1-6)
Rafiki watatu wa Ayubu washutumiwa (7-9)
Yehova ambariki tena Ayubu (10-17)
Wana na mabinti wa Ayubu (13-15)

1 Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi aliyemitwa Ayubu.^a Alikuwa mtu mnyoofu na mtimilifu;^b alimwogopa Mungu na kuepuka uovu.^c
2 Alikuwa na wana saba na mabinti watatu. **3** Mifu-

1:1 *Huenda jina hili linamaanisha “Kitu Kinachochukiwa.” ^aAu “mtu asiye na lawama na mnyoofu.”

SURA YA 1

^a Eze 14:14
Yak 5:10, 11

^b Mwa 6:9

^c Ayu 2:3

go yake ilikuwa kondoo 7,000, ngamia 3,000, ng’ombe 1,000,* na punda 500, naye alikuwa na watumishi wengi sana, na hivyo akawa mkuu kuliko watu wote wa Mashariki.

4 Kila mmoja wa wanawe alikuwa akifanya karamu kati-

1:3 *Tnn., “jozi 500 za ng’ombe.”

ka nyumba yake siku yake ili-yopangwa.* Nao walikuwa wa-kiwaalika dada zao watatu ili wale na kunywa pamoja nao. **5** Baada ya vipindi vya siku za karamu kwisha, Ayubu alikuwa akiwaita ili awatakase. Naye alikuwa akiamka asubuhi na mapema na kutoa dhabihu za kuteketezwa^a kwa ajili ya kila mmoja wao. Kwa maana Ayubu alisema: “Labda wanangu wametenda dhambi na kumtukana Mungu moyoni mwao.” Hivyo ndivyo Ayubu alivyofanya sikuzote.^b

6 Basi siku ilifika ambayo wana wa Mungu^{*c} wa kweli waliingia na kusimama mbele za Yehova,^d Shetani^e pia akaingia kati yao.^f

7 Ndipo Yehova akamuuliza Shetani: “Umetoka wapi?” Shetani akamjibu Yehova: “Nimetoka kuzururazurura na kutembeatembea duniani.”^g

8 Yehova akamwambia Shetani: “Je, umemwona* mtumishi wangu Ayubu? Hakuna yeyote aliye kama yeye duniani. Yeye ni mtu mnyoofu na mtimilifu,^{#h} anayemwogopa Mungu na kuepuka uovu.” **9** Ndipo Shetani akamjibu Yehova: “Je, Ayubu anamwogopa Mungu bure?!” **10** Je, wewe hukuweka ukuta wa ulinzi kumzunguka yeye/ na nyumba yake na kila kitu alichochacho? Umeibariki kazi ya mikono yake,^k na mifugo yake imeenea nchini. **11** Lakini, ili mambo yabadilike, nyoosha mkono wako na upige kila kitu ali-

1:4 *Au “katika nyumba ya kila mmoja kwa zamu yake.” 1:6 *Msemu wa Kiebrania unaorejelea malaika, wana wa Mungu. 1:8 *Tnn., “umeuweka moyo wako juu ya.” #Au “mtu asiye na lawama na mnyoofu.”

SURA YA 1

a Mwa 8:20
Mwa 12:7, 8

b Mwa 18:17, 19

c Mwa 6:2
Kum 33:2
Ayu 38:7d 1Fa 22:19
Zb 103:20
Da 7:13e Zek 3:1
Mt 4:1, 3
Lu 22:31
Yoh 13:2
Ufu 12:9

f Ayu 2:1-3

g 1Pe 5:8

h Mwa 6:9

i Ufu 12:10

j Mwa 15:1
Mwa 31:7

k Mwa 26:12

Safu ya 2

a Ayu 2:7

b Ayu 1:4

c Mwa 11:28

cho nacho, na kwa hakika atakutukana mbele za uso wako mwenyewe.” **12** Kisha Yehova akamwambia Shetani: “Tazama! Kila kitu alichochacho kimo mikononi mwako.* Ila tu usimnguse mwanamume huyo!” Kwa hiyo Shetani akaondoka mbele za[#] Yehova.^a

13 Sasa siku ambayo wana-we na mabinti zake walikuwa wakila na kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao mkubwa,^b **14** mjumbe akaja kwa Ayubu na kusema: “Ng’ombe walikuwa wakilima na punda walikuwa wakilisha kando yao **15** Wasabea walipotushambulia na kuwachukua, wakawau watumishi kwa upanga. Nimeponyoka mimi peke yangu, nami nimekuletea habari.”

16 Alipokuwa bado anaongea, mwingine akaja na kusema: “Moto kutoka kwa Mungu ulianguka kutoka mbinguni ukawateketeza* kabisa kondoo na watumishi! Nimeponyoka mimi peke yangu, nami nimekuletea habari.”

17 Alipokuwa bado anaongea, mwingine akaja na kusema: “Wakaldayo^c walijipanga katika makundi matatu, wakavamia ngamia na kuwachukua, nao wakawau watumishi kwa upanga. Nimeponyoka mimi peke yangu, nami nimekuletea habari.”

18 Alipokuwa bado anaongea, mwingine akaja na kusema: “Wana wako na mabinti wako walikuwa wakila na kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao mkubwa. **19** Kwa

1:12 *Au “kiko chini ya mamlaka yako.” #Tnn., “mbele za uso wa.” 1:16 *Au labda, “Radi ilianguka kutoka mbinguni ikawateketeza.”

ghafila upepo mkali ukaja kutoka nyikani, ukapiga pembe nne za nyumba hiyo, ikawaangukia vijana hao, nao wakafa. Nimeponyoka mimi peke yangu, nami nimekuletea habari.”

20 Ndipo Ayubu akasimama, akararua vazi lake na kunyoa nywele za kichwa chake; kisha akaanguka chini, akainama **21** na kusema:

“Nilitoka tumboni mwa mama yangu nikiwa uchi,

Nami nitarudi nikiwa uchi.^a

Yehova ametoa,^b na Yehova amechukua.

Jina la Yehova na liendeleo kusifiwa.”

22 Katika hayo yote, Ayubu hakutenda dhambi wala hakumlaumu Mungu kwa kutenda jambo lolote baya.*

2 Baadaye siku ilifika ambayo wana wa Mungu wa kweli*^c waliingia na kusimama mbele za Yehova,^d na Shetani pia akaingia kati yao na kusimama mbele za Yehova.^e

2 Ndipo Yehova akamuuliza Shetani: “Umetoka wapi?” Shetani akamjibu Yehova: “Nimetoka kuzururazurura na kutembea mbebe duniani.”^f

3 Yehova akamwambia Shetani: “Je, umemwona* mtumishi wangu Ayubu? Hakuna yeyote aliye kama yeye duniani. Yeye ni mtu mnyoofu na mtimilifu,^g anayemwogopa Mungu na kuepuka uovu. Bado ana-

1:22 *Au “hakusema kwamba Mungu ametenda jambo lolote lisilofaa.” 2:1 *Msemu wa Kiebrania unaorejelea malaika, wana wa Mungu. 2:3 *Tnn., “umeuweka moyo wako juu ya.” #Au “mtu asiye na lawama na mnyoofu.”

SURA YA 1

a Mwa 3:19
Zb 49:17
Mhu 5:15
Mhu 12:7
ITi 6:7

b Mhu 5:19
Yak 1:17

SURA YA 2

c Mwa 6:2
Kum 33:2
Ayu 38:7

d Zb 103:20
Da 7:13

e Ayu 1:6-8

f 1Pe 5:8

g Mwa 6:9

Safu ya 2

a Ayu 27:5

b Ayu 1:11

c Law 24:15, 16
Ayu 1:11, 12
Ufu 12:10

d Ayu 30:30

e Yer 6:26

f Ayu 1:21

g Yak 5:10, 11

h Ayu 4:1
Ayu 15:1
Ayu 22:1
Ayu 42:7, 9

i Ayu 8:1
Ayu 18:1
Ayu 25:1

j Mwa 25:1, 2

k Ayu 11:1
Ayu 20:1

shika kabisa utimilifu^a wake, hata ingawa unajaribu kuni-chochea dhidi yake^b ili nimwanguamize* bila sababu.” **4** Lakini Shetani akamjibu Yehova: “Ngozi kwa ngozi. Mtu atoa kila kitu alichu nacho ili aokoe uhai wake.* **5** Lakini, ili mambo yabadilike, nyoo-sha mkono wako upige mfupa na nyama yake, na kwa hakika atakutukana mbele za uso wako mwenyewe.”^c

6 Ndipo Yehova akamwambia Shetani: “Tazama! Yumo mikononi mwako! Ila tu usiondoe uhai wake!”* **7** Kwa hiyo Shetani akaondoka mbele za* Yehova, akampiga Ayubu kwa majipu yenye maumivu makali^d kuanzia wayo wa mguu mpaka utosini. **8** Na Ayubu akachukua kigae na kukitumia kujikuna, naye aliketiki kwenye majivu.^e

9 Hatimaye mke wake akamwambia: “Je, bado unashika kabisa utimilifu wako? Mtu-kane Mungu, ufe!” **10** Lakini akamwambia: “Unazunguma kama mmojawapo wa wana-wake wapumbavu. Je, tuku-bali tu mambo mema kutoka kwa Mungu wa kweli, tusikubali pia mambo mabaya?”^f Licha ya hayo yote, Ayubu hakutenda dhambi kwa midomo yake.^g

11 Marafiki watatu wa Ayubu wakasikia kuhusu misiba yote iliyompata Ayubu, kila mmoja wao akaja kutoka nyumbani kwake—Elifazi^h Mtemani, Bildadiⁱ Mshua,^j na Sofari^k Mnaamathi. Basi wakubaliana kukutana ili waende kumpa pole na kumfariji Ayu-

2:3 *Tnn., “nimmeze.” 2:4, 6 *Au “nafsi yake.” 2:7 *Tnn., “mbele za uso wa.” #Au “vidonda vibaya sana.”

bu. **12** Walipomwona kwa mbali, hawakumtambua. Wakaanza kulia kwa sauti kubwa na kurarua mavazi yao, wakarusha mavumbi hewani na juu ya vichwa vyao.^a **13** Kisha wakaketi ardhini pamoja naye kwa siku saba, mchana na usiku. Hakuna yeyote kati yao aliyemwambia neno lolote kwa sababu waliona kwamba alikuwa na maumivu makali sana.^b

3 Baada ya hayo Ayubu alianza kuongea na kuilaani siku aliyozaliwa.^{*c} **2** Ayubu akasema:

- 3** “Na itokomee siku niliyozaliwa,^d
Pia usiku ambao mtu alisema: ‘Mimba iliyotungwa ni ya mwanamume!’
4 Siku hiyo na iwe giza.
Mungu aliye juu asiha-
ngaikie siku hiyo;
Na nuru isiiangazie.
5 Na imilikiwe na giza zito sana.*
Wingu la mvua na litande juu yake.
Na chochote kinacholeta giza mchana kiitie hofu siku hiyo.
6 Usiku huo—na ushikwe na giza;^e
Na isishangilie miongoni mwa siku nyingine za mwaka,
Nayo isihesabiwe miongoni mwa siku za miezi.
7 Kwa kweli! Usiku huo na uwe tasa;
Kelele za shangwe zisisikiwe usiku huo.
8 Wale wanaolaani siku na wailaani,

3:1 *Tnn., “kuilaani siku yake.” 3:5 *Au “giza na kivuli cha kifo.”

SURA YA 2

a Eze 27:30, 31

b Ayu 16:6

SURA YA 3

c Yer 20:14, 15

d Ayu 10:18, 19
Yer 15:10

e Ayu 10:18, 19

Safu ya 2

a Ayu 41:1, 10
Zb 104:25, 26

b Ayu 10:18

c Yer 20:17, 18

d Mhu 9:5, 10

e Yoh 11:11

Wale wanaoweza kumwamsha Lewiathani.^{*a}

- 9** Nyota zake za alfajiri na ziwe giza;
Usiku huo ungojee nuru bila mafanikio,
Nao usione miale ya mapambazuko.
10 Kwa maana haukufunga milango ya tumbo la uzazi la mama yangu;^b
Wala haukuficha taabu kutoka machoni pangu.
11 Kwa nini sikufa nilipozaliwa?
Kwa nini sikuangamia nilipotoka tumboni?^c
12 Kwa nini mama yangu alinipakata mapajani Na kuninyonyesha?
13 Kwa maana sasa ningekuwa nimelala chini bila usumbufu;^d
Ningekuwa nimelala na kupumzika^e
14 Pamoja na wafalme wa dunia na washauri wao,
Waliojijengea majengo ambayo sasa ni magofu,*
15 Au pamoja na wakuu waliomiliki dhahabu,
Ambao nyumba zao zilijaa fedha.
16 Au kwa nini sikuwa kama mimba iliyoharibika ambayo imefichika,
Kama watoto ambao hawajawahi kamwe kuona nuru?
17 Katika kifo hata waovu hawasumbui tena;

3:8 *Inaeleweka kwamba maneno haya yanamrejilea mamba au mnyama mwingine mkubwa mwenye nguvu anayekaa ndani ya maji. 3:14 *Au labda, “Waliojijengea mahali palipo ukiwa.”

Na humo waliochoka
hupumzika.^a

- 18** Humo wafungwa hukaa pamoja kwa utulivu; Hawasikii sauti ya mtu anayewalazimisha kufanya kazi.
- 19** Humo wadogo ni sawa na wakubwa,^b Na humo mtumwa yuko huru kutoka kwa bwana wake.
- 20** Kwa nini anampa nuru anayeteseka Na kuwapa uhai wale wanaoteseka kwa uchungu mwingi?^{*c}
- 21** Kwa nini wanatamani sana kifo, lakini hakiji?^d Wanachimba wakikitafuta kuliko hazina zilizofichika,
- 22** Wale wanaoshangilia sana, Wanaofurahi wanapopata kaburi.
- 23** Kwa nini anampa nuru mwanamume aliyepotea njia, Ambaye Mungu amemzingira kwa ukuta?^e
- 24** Kwa maana badala ya chakula changu majonzi hunijia,^f Na kilio changu cha uchungu^g humwagika kama maji.
- 25** Kwa maana ninachoogopa sana kimenijia, Na ninachohofu kimenipata.
- 26** Sijawa na amani, wala utulivu, wala sijapumzika, Lakini taabu inaendelea kuniandama.”

3:20 *Au “wale walio na uchungu nafsini.”

SURA YA 3

a Zb 146:4
Mhu 9:10
Isa 57:1, 2

b Ayu 30:23
Zb 49:10, 12
Mhu 8:8
Mhu 9:2

c 1Sa 1:10
2Fa 4:27

d Hes 11:11, 15
1Fa 19:3, 4
Ayu 7:15, 16
Yon 4:2, 3

e Ayu 12:14
Ayu 19:8

f Zb 102:9, 10

g Zb 22:1
Zb 38:8

Safu ya 2

SURA YA 4

a Ayu 2:11
Ayu 15:1
Ayu 22:1
Ayu 42:7, 9

b Ayu 1:1

4 Kisha Elifazi^a Mtemani akajibu:

- 2** “Mtu akijaribu kuongea nawe, je, utakosa subira? Kwa maana ni nani anaye-weza kujizuia kuongea?
- 3** Ni kweli, umewarekebisha wengi, Nawe ulikuwa ukiimarisha mikono iliyo dhaifu.
- 4** Maneno yako yalimwinua yeyote aliyetikwa, Nawe uliwatia nguvu waliokuwa na magoti dhaifu.
- 5** Lakini sasa yamekupata wewe, nawe unalemewa;^{*} Yanakugusa, nawe unashuka moyo.
- 6** Je, hofu yako kwa Mungu haikupi ujasiri? Je, njia yako ya utimilifu^b haikupi tumaini?
- 7** Kumbuka, tafadhali: Ni mtu gani asiye na hatia ambaye amewahi kuangamia? Tangu lini wanyoofu wakaangamizwa?
- 8** Jambo ambalo nimeona ni kwamba wale wanao-lima^{*} madhara Na wale wanaopanda taabu watavuna mambo hayohayo.
- 9** Kwa pumzi ya Mungu wanaangamia, Na kwa mlipuko wa hasira yake wanafikia mwisho wao.
- 10** Simba hunguruma, na mwanasimba hurindima, Lakini hata meno ya simba wenye nguvu^{*} huvunjwa.

4:5 *Tnn., “nawe unachoka.” 4:8 *Au “wanaotunga.” 4:10 *Au “wanasimba wenye manyoya marefu shingoni.”

- 11** Simba hufa kwa kukosa mawindo,
Na wanasimba hutawanyika.
- 12** Sasa niliambiwa neno kwa siri,
Na sikio langu lilisikia mnong'ono wake.
- 13** Katika maono ya usiku yenye kufadhaisha,
Watu wanapolala usingizi mzito,
- 14** Nilitetemeka kwelikweli,
Mifupa yangu yote ikajaa hofu.
- 15** Roho fulani alipita mbele ya uso wangu;
Nywele za mwili wangu zikasimama.
- 16** Kisha akasimama tuli,
Lakini sikutambua sura yake.
Umbo fulani lilikuwa mbele ya macho yangu;
Kulikuwa na utulivu, kisha nikasikia sauti:
- 17** 'Je, mwanadamu anayeweza kufa anaweza kuwa mwadilifu kuliko Mungu? Je, mtu anaweza kuwa safi kuliko Muumba wake?'
- 18** Tazama! Hana imani na watumishi wake,
Naye huona kwamba malaika* wake wana kasoro.
- 19** Sembuse wale wanaokaa katika nyumba za udongo,
Ambao msingi wao umo mavumbini,^a
Wanaopondwa kwa urahisi kama nondo!*
- 20** Wanapondwa kabisa kuanzia asubuhi mpaka jioni;

4:18 *Au "wajumbe." 4:19 *Aina fulani ya wadudu waharibifu.

SURA YA 4

a Mwa 3:19

Safu ya 2

SURA YA 5

a Met 22:22
Amo 5:12

- Wanaangamia milele, na hakuna yeyote anayetambua hilo.
- 21** Je, wao si kama hema ambalo kamba yake imeng'olewa?
Wanakufa bila hekima.
- 5** "Ita, tafadhali! Je, kuna yeyote anayekujibu? Ni mtakatifu gani utakayemlilia?"
- 2** Kwa maana kinyongo kitamuua mpumbavu,
Na wivu utamwangamiza mjinga.
- 3** Nimemwona mpumbavu akitia mizizi,
Lakini kwa ghafla makao yake yanalaaniwa.
- 4** Wanawe hawana usalama wowote,
Nao hupondwa kwenye lango la jiji,^a na hakuna yeyote wa kuwaokoa.
- 5** Mwenye njaa hula anachovuna,
Hukichukua hata katikati ya miiba,
Na mtego umetegwa ili kunasa mali zao.
- 6** Kwa maana mambo yenye kudhuru hayaoti mavumbini,
Na taabu haichipuki ardhini.
- 7** Kwa maana mwanadamu huzaliwa ili ataabike,
Hilo ni hakika kama cheche za moto zinavyoruka juu.
- 8** Lakini mimi ningemsihi Mungu,
Nami ningewasilisha kesi yangu kwa Mungu,
- 9** Kwa Yule anayetenda mambo makuu na yasiyochunguzika,

Mambo yenye kustaajabi-
sha yasiyohesabika.

- 10** Yeye huleta mvua duniani
Na kupeleka maji masha-
mbani.
- 11** Humwinua juu mtu wa hali
ya chini,
Humwinua aliyehuzunika
na kumwoko.
- 12** Huvuruga njama za wenye
hila,
Ili kazi ya mikono yao
isifanikiwe.
- 13** Huwanasa wenye hekima
katika ujanja wao
wenyewe,^a
Hivi kwamba mipango
ya watu werevu huvu-
rugika.
- 14** Wao hukutana na giza
wakati wa mchana,
Nao hupapasa-papasa
wakati wa aduhuri
kana kwamba ni usiku.
- 15** Huokoa kutokana na
upanga wa kinywa chao,
Humwoko maskini
kutoka katika mkono
wa mwenye nguvu,
- 16** Hivi kwamba kuna
tumaini kwa mtu wa
hali ya chini,
Lakini kinywa cha uovu
hufumbwa.
- 17** Tazama! Mwenye furaha
ni mtu ambaye Mungu
humkaripia;
Basi usikatae nidhamu ya
Mweza-Yote!
- 18** Kwa maana yeye husa-
babisha maumivu, lakini
hufunga jeraha;
Huvunja, lakini huponya
kwa mikono yake.
- 19** Atakuokoa katika misiba
sita,
Hata wa saba hautaku-
dhuru.

SURA YA 5

a 1Ko 3:19

Safu ya 2

a Met 12:18

SURA YA 6

b Zb 31:9

- 20** Wakati wa njaa kali
atakukomboa kutoka
katika kifo,
Na kutoka katika nguvu za
upanga wakati wa vita.
- 21** Utalindwa dhidi ya
mashambulizi ya ulimi,^a
Nawe hutaogopa uharibifu
utakapokuja.
- 22** Utacheke maangamizi na
njaa,
Wala hutawaogopa wanya-
ma wa mwituni walio
duniani.
- 23** Kwa maana mawe ya sha-
mbani hayatakudhuru,*
Na wanyama wa mwituni
wataishi nawe kwa
amani.
- 24** Utajua kwamba hema lako
liko salama,*
Na hakuna kitakachoko-
sekana utakapokagua
malisho yako.
- 25** Utakuwa na watoto wengi,
Na wazao wako watakuwa
wengi kama mimea du-
niani.
- 26** Utaingia kaburini ukiwa
bado na nguvu,
Kama masuke ya nafaka
yanayokusanywa wakati
wa mavuno.
- 27** Tazama! Tumechunguza
jambo hili, na ndivyo
lilivyo.
Sikiliza na ulikubali.”
- 6** Kisha Ayubu akajibu:
2 “Laiti maumivu yangu
makali^b yangepimwa
kikamili
Na kuwekwa kwenye
mizani pamoja na
msiba wangu!
3 Kwa maana sasa ni mazito

5:23 *Au “yatafanya agano (mapatano)
nawe.” 5:24 *Tnn., “ni amani.”

kuliko mchanga wa bahari.

Ndiyo sababu maneno yangu yamekuwa mazungumzo ya ovyoovy. ^{*a}

4 Kwa maana mishale ya Mweza-Yote imenichoma,

Na roho yangu inakunywa sumu yake;^b

Vitisho vya Mungu vinaniandama.

5 Je, punda mwtu^c atalia akiwa na majani, Au ng'ombe dume atalia akiwa na chakula?

6 Je, chakula kisicho na ladha huliwa bila chumvi, Au maji ya mholi yana ladha?

7 Nimekataa kugusa vitu vya aina hiyo. Ni kama uchafu katika chakula changu.

8 Laiti ombi langu lingebiwiwa Na laiti Mungu angenipa ninachotamani!

9 Kwamba Mungu angekuwa tayari kunipondaponda, Na kwamba angeunyoosha mkono wake na kuniangamiza!^d

10 Kwa maana hata hilo lingenifariji; Ningeruka kwa shangwe licha ya maumivu yangu yasiyokwisha, Kwa maana sijayakana maneno ya Aliye Mtakatifu.^e

11 Je, nina nguvu za kuendelea kungoja?^f Na ni mwisho gani unao-nisubiri, hivi kwamba niendeleo kuishi?*

6:3 *Au "nimezungumza bila kufikiri; harakaharaka." 6:11 *Au "hivi kwamba nirefushe maisha yangu (nafsi yangu)?"

SURA YA 6

a Mhu 7:7
Yak 3:2

b Met 18:14

c Ayu 24:5

d Hes 11:11, 15
1Fa 19:3, 4
Yon 4:3

e Law 19:2
Ho 11:9

f Ayu 7:6, 7
Zb 103:15, 16

Safu ya 2

a Met 3:3
Met 19:22
Ho 6:6
Zek 7:9

b 1Yo 3:17

c Ayu 19:19
Zb 38:11

d Isa 21:13, 14

e Ayu 1:14, 15

f Ayu 13:4

12 Je, nguvu zangu ni kama za mwamba? Au mwili wangu umetengezwa kwa shaba?

13 Je, kuna njia yoyote ninayoweza kujisaidia mwenyewe Wakati nimenyang'anywa njia zangu zote za kujitegemeza?

14 Yeyote anayekataa kumtendea mwanadamu mwenzake kwa upendo mshikamanifu^a Ataacha kumwogopa Mweza-Yote.^b

15 Ndugu zangu wenyewe wamekuwa na hila^c kama kijito cha majira ya baridi kali,

Kama maji ya vijito vya majira ya baridi kali yanayokauka.

16 Vimekuwa vyeusi kwa sababu ya barafu, Na theluji inayoyeyuka imejificha ndani yake.

17 Lakini katika majira ya kiangazi vinakauka na kutoweka; Joto linapoongezeka, vinakauka.

18 Mikondo yake hugeuka; Navyo huelekea jangwani na kutoweka.

19 Misafara ya Tema^d huvitafuta; Wasafiri kutoka Sheba^{*e} huvingojea.

20 Wameaibika kwa sababu hawakupata walichotumaini; Wanafika hapo na kukata tamaa tu.

21 Hivyo ndivyo mlivyo kwangu mimi;^f

6:19 *Au "Msafara wa Wasabea."

- Mmeona mateso ya msiba wangu, nanyi mnaogopa.^a
- 22** Je, nimewaambia, 'Nipeni kitu fulani,'
Au kuwaomba zawadi yoyote kutoka katika mali zenu?
- 23** Je, nimeomba niokolewe kutoka mikononi mwa adui
Au niokolewe* kutoka kwa wakandamizaji?
- 24** Nifundisheni, nami nita-nyamaza;^b
Nisaidieni kuelewa kosa langu.
- 25** Maneno ya unyoofu hayaumizi!^c
Lakini karipio lenu lina faida gani?^d
- 26** Je, mnapanga njama ya kukosoa maneno yangu,
Maneno ya mtu aliyekata tamaa,^e yanayopeperushwa mbali na upepo?
- 27** Ninyi hata mngeweza kupiga kura kwa ajili ya yatima^f
Na kumuza rafiki yenu!^g
- 28** Basi sasa geukeni mmitazame,
Kwa maana siwezi kusema uwongo mbele yenu.
- 29** Fikirieni tena, tafadhali—msinielewe vibaya—
Naam, fikirieni tena, kwa maana mimi bado ni mwadilifu.
- 30** Je, ulimi wangu unasema jambo lisilo la haki?
Je, mdomo wangu haitambui* kwamba kuna jambo ambalo si sawa?

6:23 *Tnn., "nikombolewe." 6:27 *Au "kubadilishana rafiki yenu kwa mali." 6:30 *Tnn., "kaakaa langu halitambui."

SURA YA 6

a Zb 38:11

b Ayu 32:11, 12

c Met 12:18
Met 25:11d Ayu 16:2, 3
Ayu 21:34

e Ayu 10:1

f Ayu 31:21, 22
Mal 3:5

g Mwa 37:28

Safu ya 2

SURA YA 7

a Ayu 14:5, 6
Zb 39:4b Law 19:13
Kum 24:15

c Zb 6:6

d Ayu 2:8
Ayu 30:17

e Ayu 30:19

f Ayu 30:30

g Zb 102:11
Zb 103:15
Zb 144:4

h Ayu 17:15

i Zb 89:47
Mhu 2:11j Ayu 7:21
Yak 4:14k Ayu 10:21
Ayu 14:12
Zb 78:39
Mhu 9:10

- 7** "Je, maisha ya mwanadamu anayeweza kufa si kama kazi ya kulazimishwa,
Na siku zake kama siku za kibarua?"^a
- 2** Kama mtumwa, anatamani sana kivuli,
Na kama kibarua, anasubiri mshahara wake.^b
- 3** Kwa hiyo nimepangiwa miezi ya ubatili
Nami nimehesabiwa usiku baada ya usiku wa kuteseka.^c
- 4** Ninapolala mimi huuliza, 'Nitaamka wakati gani?'^d
Lakini kadiri usiku unavyojikokota, ndivyo ninavyogaagaa hadi alfajiri.*
- 5** Mwili wangu umefunikwa na mabuu na magamba ya uchafu;^e
Ngozi yangu imejaa vigaga na usaha.^f
- 6** Siku zangu zinasonga upesi sana kuliko gurudumu la mfumaji,^g
Nazo zinafikia mwisho bila tumaini.^h
- 7** Kumbukeni kwamba maisha yangu ni upepo,ⁱ
Kwamba jicho langu halitaona tena kamwe furaha.*
- 8** Jicho linaloniona sasa halitaniona tena;
Macho yenu yatanitafuta, lakini nitakuwa nimeenda zangu.^j
- 9** Kama wingu linalofikia kutoweka,
Mtu anayeshuka chini Kaburini* harudi juu tena.^k

7:4 *Au "mpaka mapambazuko." 7:7 *Tnn., "mema." 7:9 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

- 10** Hatarudi tena katika nyumba yake, Na mahali pake hapata-mtambua tena.^a
- 11** Kwa hiyo, sitazuia kinywa changu. Nitaongea kwa uchungu wa roho yangu; Nitalalamika katika mate-so yangu makali!^{*b}
- 12** Je, mimi ni bahari au mnyama mkubwa sana wa baharini, Hivi kwamba uniwekee mlinzi?
- 13** Ninaposema, 'Kochi langu litanifariji; Kitanda changu kitasaidia kupunguza mateso yangu,'
- 14** Kisha unanitisha kwa ndoto Na kuniogopesha kwa maono,
- 15** Hivi kwamba natamani kusongwa pumzi, Naam, natamani kifo bada-la ya mwili huu wangu.^{*c}
- 16** Ninachukia maisha yangu;^d sitaki kue-ndelea kuishi. Niche, kwa maana siku zangu ni kama pumzi.^e
- 17** Mwanadamu anayeweza kufa ni nini hivi kwamba umhangaikie Na kumkazia uangalifu?^{*f}
- 18** Kwa nini unamkagua kila asubuhi Na kumjaribu kila wakati?^g
- 19** Je, hutaacha kunitazama Na kuniacha peke yangu nipate muda wa kumeza mate?^h

7:11 *Au "kwa uchungu wa nafsi yangu!"
7:15 *Tnn., "badala ya mifupa yangu."
7:17 *Tnn., "kuuweka moyo wako juu yake?"

SURA YA 7

a Zb 103:15, 16
Zb 146:4
Mhu 9:5

b 1Sa 1:10
Ayu 10:1
Met 14:10

c Ayu 3:20, 21

d Mwa 27:46
1Fa 19:4
Ayu 10:1
Yon 4:3

e Zb 62:9
Zb 144:4
Mhu 6:12

f Zb 8:4
Zb 103:15
Zb 144:3

g Ayu 23:10

h Ayu 14:6

Safu ya 2

a Ayu 34:21
Met 5:21
Yer 16:17
Ebr 4:13
1Pe 3:12

b Mwa 3:19
Zb 104:29
Mhu 12:7

SURA YA 8

c Ayu 18:1
Ayu 25:1

d Mwa 25:1, 2
Ayu 42:9

e Ayu 11:3

f Ayu 5:8, 9
Ayu 11:13
Ayu 22:23

g Ayu 1:8

h Ayu 11:14, 17

- 20** Ikiwa nimetenda dhambi, ninawezaje kukudhuru wewe, Mchunguzaji wa wanadamu?^a

Kwa nini umenifanya niwe shabaha yako?
Je, nimekuwa mzigo kwako?

- 21** Kwa nini husamehi dhambi yangu Na kuachilia kosa langu? Kwa maana hivi punde nitalala mavumbini,^b Nawe utanitafuta, lakini nitakuwa nimeenda zangu."

8

Kisha Bildadi^c Mshua^d akajibu:

- 2** "Utaendelea kuongea kwa njia hiyo mpaka lini?^e Maneno ya kinywa chako ni upepo wenye nguvu!
- 3** Je, Mungu atapotosha haki, Au, je, Mweza-Yote atapotosha uadilifu?
- 4** Ikiwa watoto wako walimtendea dhambi, Aliwaacha waadhibiwe kwa sababu ya uasi wao;*
- 5** Laiti ungemtumaini Mungu^f Na kumsihi Mweza-Yote upate kibali chake,
- 6** Na ikiwa kwa kweli ungekuwa safi na mnyoofu,^g Angekusikiliza* Na kukurudisha mahali unapostahili.
- 7** Na ingawa mwanzo wako ulikuwa mdogo, Wakati wako ujao utakuwa mkubwa.^h

8:4 *Tnn., "Aliwatia mikononi mwa uasi wao." 8:6 *Tnn., "Angeinuka kwa ajili yako."

- 8** Tafadhali, uliza kizazi kilichotangulia,
Na usikilize mambo ambayo baba zao walijifunza.^a
- 9** Kwa maana tulizaliwa jana tu, nasi hatujui lolote, Kwa sababu siku zetu duniani ni kivuli.
- 10** Je, hawatakufundisha Na kukwambia wanayojua?*
- 11** Je, mafunjo yanaweza kusitawi katika eneo lisilo na umajimaji?
Je, utete unaweza kusitawi bila maji?
- 12** Hata kabla haujachanua, kabla haujakatwa, Utakauka kabla ya mmea mwingine wowote.
- 13** Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa* wote wanaomsahau Mungu, Kwa maana tumaini la wanaomkataa Mungu# litapotea,
- 14** Ambao tegemeo lao ni ubatili
Na ambao tumaini lao ni hafifu kama utando wa* buibui.
- 15** Ataegemea nyumba yake, lakini haitaendelea kusimama;
Atajaribu kuishikilia, lakini haitadumu.
- 16** Yeye ni mmea wenye unyenyevu juani,
Na matawi yake huenea shambani.^b
- 17** Mizizi yake husokotana katika rundo la mawe; Hutafuta nyumba katikati ya mawe.*

8:10 *Tnn., "Na kusema maneno yaliyo moyoni mwao?" **8:13** *Tnn., "Hivyo ndivyo zilivyo njia za." #Au "wasisi imani." **8:14** *Tnn., "nyumba ya." **8:17** *Au "Hutazama nyumba ya mawe."

SURA YA 8

a Ayu 15:17,18

b Ayu 5:3

Safu ya 2

a Ayu 20:9

b Ayu 20:5

SURA YA 9

c Kum 32:4
Zb 143:1,2
Ro 3:23d Ayu 40:2
Ro 9:20e Ayu 36:5
Zb 104:24
Isa 40:26
Da 2:20f Met 14:16
Met 28:14
Isa 30:1
Da 5:18,20
Zek 7:12
Ro 2:5

- 18** Lakini anapong'olewa* kutoka mahali pake, Mahali hapo patamkana na kusema, 'Sijawahi kamwe kukuona.'^a
- 19** Naam, hivyo ndivyo atakavyotoweka,*^b
Kisha wengine watachipuka kutoka mavumbini.
- 20** Kwa hakika Mungu hatawakataa watu wanaoshika utimilifu;* Wala hatawaunga mkono# waovu,
- 21** Kwa maana bado atakijaza kinywa chako kicheko Na midomo yako kelele za shangwe.
- 22** Wale wanaokuchukia watawishwa aibu, Na hema la waovu halitakuwapo tena."
- 9** Ayubu akajibu:
- 2** "Kwa kweli ninajua hivyo ndivyo ilivyo. Lakini mwanadamu anayeweza kufa anawezaje kuwa mwadilifu katika kesi na Mungu?^c
- 3** Mtu akitaka kubishana Naye,*^d
Mtu huyo hawezi kujibu hata swali moja kati ya maswali Yake elfu moja.
- 4** Yeye ni mwenye hekima moyoni na ana nguvu nyingi sana.^e
Ni nani anayeweza kumpinga na asipate madhara?^f
- 5** Yeye huihamisha* milima bila yeyote kujua;

8:18 *Au "anapomezwa." **8:19** *Au "hivyo ndivyo njia yake itakavyoyeyuka." **8:20** *Au "wasio na lawama." #Tnn., "hatawashika mkono." **9:3** *Au "kumpeleka mahakamani." **9:5** *Au "huiondoa."

Huipindua kwa hasira yake.

- 6** Huitikisa dunia kutoka mahali pake, Hivi kwamba nguzo zake zinatetemeka.^a
- 7** Huliamura jua lisiangaze Naye huziba kabisa nuru ya nyota;^b
- 8** Huzitandaza mbingu akiwa peke yake,^c Naye hukanyaga mawimbi makubwa ya bahari.^d
- 9** Aliumba kundi la nyota la Ashi,* Kesili,# na Kima,^{△e} Na makundi ya nyota yaliyo katika anga la kusini;[⊞]
- 10** Hufanya mambo makuu yasiyochunguzika,^f Mambo yenye kustaajabisha yasiyoweza kuhesabiwa.^g
- 11** Yeye hupita karibu nami, lakini siwezi kumwona; Hupita mbele yangu, lakini siwezi kumtambua.
- 12** Anapochukua kitu kwa ghafla, ni nani anayeweza kumzuia? Ni nani anayeweza kumuuliza, 'Unafanya nini?'^h
- 13** Mungu hataizuia hasira yake;ⁱ Hata wanaomsaidia Raha-bu*^j watamwinamia.
- 14** Sembuse ninapomjibu Ni lazima nichague maneno yangu kwa uangalifu ili kujadiliana naye!

9:9 *Labda ni kundi la nyota la Dubu Mkubwa (Kundi Kubwa la Ursa). ^aLabda ni kundi la nyota la Orioni. [△]Labda ni nyota zinazoitwa Pleiadesi katika kundi la nyota la Taurusi, au Ng'ombe. [⊞]Tnn., "katika vyumba vya ndani vya kusini." **9:13** *Labda ni mnyama mkubwa sana wa baharini.

SURA YA 9

a Zb 75:3

b Mwa 1:16

c Mwa 1:1
Zb 33:6
Isa 44:24

d Ayu 38:8-11

e Ayu 38:31
Amo 5:8f Isa 40:28
Ro 11:33

g Zb 40:5

h Da 4:35
Ro 9:20

i Kum 32:22

j Ayu 26:12

Safu ya 2

a Ayu 10:15

b Ayu 2:3
Ayu 34:5, 6

c Isa 40:28

d 1Yo 5:19

- 15** Hata kama singekuwa na kosa, singemjibu.^a Ningemsihi tu mwamuzi* wangu anionyeshe rehema.
- 16** Nikimwita, je, atanijibu? Siamini kwamba atasikiliza sauti yangu,
- 17** Kwa maana yeye huniponda kwa dhoruba Naye huzidisha majeraha yangu bila sababu.^b
- 18** Haniruhusu nipumue; Huendelea kunjijaza mambo machungu.
- 19** Kama ni nguvu, yeye ndiye mwenye nguvu.^c Kama ni haki, anauliza: 'Ni nani anayeweza kuni-shtaki?'
- 20** Kama singekuwa na kosa, kinywa changu mwenyewe kingenishutumu; Hata nikishika utimilifu wangu,* atanitangaza kuwa mwenye hatia.[#]
- 21** Hata nikishika utimilifu wangu,* sijiamini;[#] Ninakataa[△] maisha haya yangu.
- 22** Yote ni sawa. Ndiyo saba-bu ninasema, 'Yeye huwaangamiza wasio na hatia* na waovu pia.'
- 23** Mafuriko ya ghafla yakisababisha kifo ghafla, Ataidhihaki hali ya kukata tamaa ya watu wasio na hatia.
- 24** Dunia imetiwa mikononi mwa mwovu;^d

9:15 *Au labda, "mshtaki." **9:19** *Tnn., "kunipeleka mahakamani?" **9:20** *Au "Hata nikiwa bila hatia." [#]Tnn., "atanitangaza kuwa mpotovu." **9:21** *Au "nikiwa bila hatia." [#]Au "Sijui nafsi yangu." [△]Au "Ninadharau." **9:22** *Au "watimilifu."

- Huwafumba macho*
waamuzi wake.
Kama si yeye, ni nani basi?
- 25 Sasa siku zangu zina-
kimbia kasi kuliko
mkimbiaji;^a
Zinakimbia na kutoweka
bila kuona mema.
- 26 Zinanyiririka kama
mashua za matete,
Kama tai wanaoshuka kwa
ghafila kukamata mawi-
ndo yao.
- 27 Nikisema, 'Nitasahau
malalamiko yangu,
Nitabadili hali ya uso
wangu na kuwa
mchangamfu,'
- 28 Bado nitaogopa kwa sa-
babu ya maumivu yangu
yote,^b
Nami najua hutanipata
bila hatia.
- 29 Nitapatikana na hatia.*
Basi kwa nini nitaabike
bure?^c
- 30 Nikioga kwa maji ya thelu-
ji inayoyeyuka,
Na kunawa mikono yangu
kwa sabuni,^{*d}
- 31 Wewe utanitumbukiza
shimoni,
Hivi kwamba hata mavazi
yangu mwenyewe yatani-
chukia.
- 32 Kwa maana yeye si mwa-
nadamu kama mimi ili
nimjibu,
Hivi kwamba twende
mahakamani pamoja.^e
- 33 Hakuna mtu wa kuamua
kesi baina yetu wawili,*
Anayeweza kuwa mwamu-
zi wetu.[#]

9:24 *Tnn., "nyuso." 9:29 *Tnn., "kuwa mwovu." 9:30 *Au "magadi." 9:33 *Au "kutupatanisha." #Tnn., "kuweka mkono wake juu yetu wawili."

SURA YA 9

a Ayu 7:6
Zb 90:10
Yak 4:14

b Ayu 21:6

c Zb 73:13

d Yer 2:22
Mal 3:2

e Isa 45:9
Ro 9:20

Safu ya 2

a Ayu 13:21

SURA YA 10

b Hes 11:11, 15
1Fa 19:3, 4
Ayu 7:16
Yon 4:3

c Ayu 14:15
Zb 138:8
Isa 64:8

d Zb 90:2

e Ayu 10:14

f Ayu 1:8
Zb 139:1

g Kum 32:39

34 Ikiwa angeacha kunipiga*
Na kuacha kuniogopesha
kwa vitisho vyake,^a

35 Ndipo ningeongea naye
bila woga,
Kwa sababu sijazoea kuo-
ngea kwa woga.

10 "Nayachukia sana* mai-
sha yangu.^b

Nitamwaga malalamiko
yangu.

Nitasema waziwazi katika
mateso yangu makali![#]

2 Nitamwambia Mungu:
'Usinitangaze kuwa
mwenye hatia.

Niambie kwa nini unapa-
mbana nami.

3 Je, unafaidika unaponika-
ndamiza,

Unapodharau kazi ya mi-
kono yako^c

Huku ukipendelea ushauri
wa waovu?

4 Je, una macho ya kimwili,
Au je, unaona kama mwa-
nadamu anayeweza kufa
anavyoona?

5 Je, siku zako ni kama siku
za wanadamu wanaowe-
za kufa,

Au je, miaka yako ni kama
ya mwanadamu,^d

6 Hivi kwamba utafute
kosa langu
Na kuendelea kutafuta
dhambi yangu?^e

7 Unajua kwamba sina
hatia;^f

Na hakuna yeyote ana-
yeweza kuniokoa kutoka
mkononi mwako.^g

8 Mikono yako mwenyewe

9:34 *Tnn., "angeondoa fimbo yake juu yangu." 10:1 *Au "Nafsi yangu inachukia sana." #Au "kwa uchungu mwingi sana wa nafsi yangu!"

- ilinfinyanga na kuni-
umba,^a
Lakini sasa unataka kunia-
ngamiza kabisa.
- 9** Tafadhali, kumbuka
kwamba uliniumba
kwa udongo,^b
Lakini sasa unanirudisha
mavumbini.^c
- 10** Je, hukunimwaga kama
maziwa
Na kunigandisha kama ji-
bini?
- 11** Ulinivisha ngozi na
nyama,
Na kunifuma kwa mifupa
na misuli.^d
- 12** Umenipa uhai na kunipe-
nda kwa ushikamanifu;
Umeilinda na kuitunza
roho yangu.^e
- 13** Lakini ulikusudia kwa siri
kufanya mambo haya.*
Najua kwamba mambo
haya yametoka kwako.
- 14** Ikiwa ningetenda dhambi,
ungenitazama,^f
Nawe hungenisamehe kosa
langu.
- 15** Kama nina hatia, ole wa-
ngu!
Na hata kama sina hatia,
siwezi kuinua kichwa
changu,^g
Kwa sababu nimejaa aibu
na mateso.^h
- 16** Nikiinua kichwa changu
juu, unaniwinda kama
simbaⁱ
Na kuonyesha tena nguvu
zako dhidi yangu.
- 17** Unaleta mashahidi wapya
dhidi yangu
Na kuzidisha hasira yako
dhidi yangu,

10:12 *Au "pumzi yangu; uhai wangu."

10:13 *Tnn., "Na mambo haya umeyafi-
cha moyoni mwako."

SURA YA 10

a Zb 119:73
Zb 139:13-16

b Mwa 2:7
Isa 45:9
Isa 64:8
Ro 9:21

c Mwa 3:19
Zb 104:29
Mhu 12:7

d Zb 139:15

e Zb 8:4

f Zb 139:1

g Ayu 9:15

h Zb 119:153

i Isa 38:13

Safu ya 2

a Ayu 3:11
Yer 20:18

b Ayu 7:6
Ayu 14:1, 2
Zb 39:5, 6
Zb 103:15, 16

c Ayu 9:27

d Ayu 7:9
Zb 115:17
Isa 38:11

e Ayu 38:17
Zb 88:12
Mhu 9:10

SURA YA 11

f Ayu 20:1
Ayu 42:9

g Ayu 12:4

h Ayu 6:10

Huku shida baada ya shida
ikinikabili.

- 18** Basi kwa nini ulinitoa
katika tumbo la mama
yangu?^a
Laiti ningekufa kabla ya
jicho lolote kuniona.
- 19** Ingekuwa kana kwamba
sikuwahi kuwepo;
Ningetolewa moja kwa
moja tumboni na kupe-
lekwa kaburini.[']
- 20** Je, siku zangu si chache?^b
Naomba aniache;
Na ayageuze macho yake
mbali nami, ili nipate
kitulizo kidogo.*^c
- 21** Kabla sijaenda zangu
—nami sitarudi^d—
Katika nchi yenye giza zito
kabisa,^{*e}
- 22** Kwenye nchi yenye giza
totoro,
Nchi ya kivuli kizito na vu-
rugu,
Ambako hata nuru ni
kama giza."
- 11** Sofari^f Mnaamathi
akajibu:
- 2** "Je, maneno haya yote
yatakosa kujibiwa,
Au kuongea mengi kuta-
mfanya mtu asiwe na
kosa?*
- 3** Je, maneno yako yasiyo
na maana yatawanyama-
zisha watu?
Unadhani hakuna ataka-
yekukemea kwa sababu
ya maneno yako ya
dhihaka?^g
- 4** Kwa sababu unasema,
'Mafundisho yangu ni
safi,^h
- 10:20** *Au "nichangamke kidogo."
10:21 *Au "yenye giza na kivuli cha
kifo." **11:2** *Au "mwenye kujigamba
atakuwa bila kosa?"

Nami niko safi machoni pako.^a

- 5** Lakini laiti Mungu angezu-ngumza
Na kukufungulia midomo yake!^b
- 6** Ndipo angekufunulia siri za hekima,
Kwa maana hekima inayotumika ina vipengele vingi.
Kisha ungetambua kwa mba Mungu huruhusu baadhi ya makosa yako yasahauliwe.
- 7** Je, unaweza kugundua mambo ya Mungu yenye kina
Au kugundua kila jambo kumhusu * Mweza-Yote?
- 8** Hekima yake iko juu kuliko mbingu. Wewe unaweza kutimiza nini?
Ina kina kuliko Kaburi. *
Wewe unaweza kujua nini?
- 9** Ni ndefu kuliko dunia
Na pana kuliko bahari.
- 10** Akipita na kumkamata mtu na kuweka kikao cha mahakama,
Ni nani anayeweza kumpinga?
- 11** Kwa maana anajua watu wanapokuwa wadangan-yifu.
Akiona uovu, je, hatautambua?
- 12** Lakini mtu asiye na akili ataelewa
Wakati tu punda mwitu atakapoweza kuzaa mwanadamu.*

11:7 *Au "mipaka ya." **11:8** *Au "Sheo-li." Angalia Kamusi, uku. 2012. **11:12** *Au "Wakati tu punda mwitu atakapozaliwa akiwa mwanadamu."

SURA YA 11

^a Ayu 6:29
^b Ayu 10:7

- 13** Laiti ungeutayarisha moyo wako
Na kunnyooshea mikono yako.
- 14** Ikiwa mkono wako unatenda mabaya, utupilie mbali,
Nawe usiruhusu uovu ukae katika mahema yako.
- 15** Ndipo utakapoinua uso wako bila lawama;
Utaweza kusimama imara, bila woga.
- 16** Ndipo utakapoisahau taabu yako;
Utaikumbuka kama maji yaliyopita karibu nawe na kwenda zake.
- 17** Maisha yako yatang'aa kuliko adhuhuri;
Hata giza lake litakuwa kama asubuhi.
- 18** Utakuwa na ujasiri kwa sababu kuna tumaini,
Nawe utatazama huku na huku na kulala kwa usalama.
- 19** Utalala na hakuna yeyote atakayekuogopesha,
Na watu wengi watajipendekeza kwako.
- 20** Lakini macho ya waovu yatadhoofika;
Nao hawatapata mahali pa kukimbilia,
Na tumaini lao pekee litakuwa kifo."^a
- 12** Kisha Ayubu akajibu:
2 "Kwa kweli ninyi ndio mnaojua,*
Na hekima itakufa pamoja nanyi!
3 Lakini mimi pia nina uelewaji.*
Mimi si duni kwenu.

^b Ayu 38:1

Safu ya 2

^a Ayu 8:13,14
^b Ayu 18:5,14

12:2 *Tnn., "ninyi ndio watu." **12:3** *Tnn., "moyo."

- Ni nani asiyejua mambo haya?
- 4** Nimekuwa kichekesho kwa rafiki zangu,^a
Mtu anayemlilia Mungu ili amjibu.^b
Mtu mwadilifu na asiye na lawama ni kichekesho.
- 5** Mtu asiye na mahangaiko hudharau msiba, Akifikiri kwamba msiba huwajia tu wale ambao miguu yao inayumba-yumba.*
- 6** Mahema ya wezi yana amani,^c
Na wale wanaomkasirisha Mungu wako salama,^d
Wale wanaobeba mungu wao mikononi mwao.
- 7** Lakini, tafadhali, waulize wanyama, nao watakufundisha;
Pia ndege wa angani, nao watakwambia.
- 8** Au ichunguze* dunia, nayo itakufundisha;
Na samaki wa baharini watakutangazia.
- 9** Ni nani kati ya hao wote asiyejua
Kwamba mkono wa Yehova umefanya haya?
- 10** Uhai wa kila kiumbe umo* mikononi mwake
Na roho# ya kila mwana-damu.^e
- 11** Je, sikio halipimi maneno Kama ulimi unavyoonja* chakula?^f
- 12** Je, hekima haipatikani miongoni mwa waliozeeka,^g
Na je, uelewaji hauji kwa

12:5 *Au "inateleza." 12:8 *Au labda, "zungumza na." 12:10 *Au "Nafsi ya kila mtu aliye hai imo." #Au "pumzi." 12:11 *Tnn., "kaakaa linavyoonja."

SURA YA 12

a Ayu 16:10
Ayu 17:2
Ayu 30:1
Zb 22:7
Ebr 11:36

b Zb 91:15
Mik 7:7

c Zb 37:35
Zb 73:12
Yer 12:1

d Ayu 21:7,9

e Hes 16:22
Zb 104:30
Mhu 12:7
Eze 18:4

f Ayu 34:3

g Ayu 32:6,7

Safu ya 2

a Ayu 9:4
Da 2:20

b Ayu 36:5
Zb 147:5
Isa 40:14
Yer 10:12
Ro 11:34

c Yud 7

d Mwa 8:1
Kut 14:21
Nah 1:4

e Mwa 6:17

f Ro 1:20

g Isa 29:14
Isa 44:25

h Da 2:21

i Yer 14:18

j Lu 1:52

k Zb 107:40

l Da 2:22

sababu ya kuishi muda mrefu?

- 13** Yeye ana hekima na nguvu;^a
Ana mashauri na uelewaji.^b
- 14** Anapobomoa kitu, hakiwezi kujengwa tena;^c
Alichofunga, hakuna mwanaadamu anayeweza kukifungua.
- 15** Anapoyazuia maji, kila kitu hukauka;^d
Anapoyaachilia, yanailemea dunia.^e
- 16** Ana nguvu na hekima inayotumika;^f
Anayepotosha na anayepotoshwa wote ni wake;
- 17** Huwafanya washauri watembee bila viatu,^{*}
Naye huwafanya waa-muzi waonekane wapumbavu.^g
- 18** Hulegeza pingu zilizofungwa na wafalme,^h
Naye huwafunga mshipi kiunoni.
- 19** Huwafanya makuhani watembee bila viatu,ⁱ
Naye huwapindua walio imara kabisa katika mamlaka;^j
- 20** Huwanyamazisha washauri wanaotegemeka
Na kuwapokonya wanau-me wazee* busara;
- 21** Huwamwagia wakuu dharaui,^k
Naye huwafanya wenye nguvu wawe dhafu;^{*}
- 22** Hufunua mambo yenye kina kutoka gizani,^l
Naye huleta giza zito kwenye nuru;

12:17 *Au "bila chochote." 12:20 *Au "wazee." 12:21 *Tnn., "hulegeza mshipi wa wenye nguvu."

- 23** Huyafanya mataifa yawe na nguvu ili ayaangamize;
Huyafanya mataifa yawe makubwa ili ayapeleke uhamishoni.
- 24** Huwapokonya viongozi wa watu uelewaji* wao
Na kuwafanya watangeta-nge jangwani kusiko na njia.^a
- 25** Wao hupapasa-papasa gizani,^b ambamo hamna nuru;
Huwafanya wapepesuke kama walevi.^c
- 13** “Naam, jicho langu limeona hayo yote, Sikio langu limesikia na kuyaelewa.
- 2** Mnayojua, mimi pia nayajua;
Mimi si duni kwenu.
- 3** Lakini mimi, ni afadhali nizungumze na Mweza-Yote mwenyewe;
Ninatamani kujitetea mbele za Mungu.^d
- 4** Lakini ninyi mnanipaka uwongo;
Ninyi nyote ni matabibu wasiofaa kitu.^e
- 5** Laiti mngenyamaza kabisa,
Mngeonekana kuwa wenye hekima.^f
- 6** Tafadhali, sikilizeni hoja zangu,
Na msikilize ninapojitetea kwa midomo yangu.
- 7** Je, mtasema mambo yasiyo ya haki kwa niaba ya Mungu,
Na je, mtazungumza kwa udanganyifu kwa ajili yake?

12:24 *Tnn., “moyo.”

SURA YA 12

a Zb 107:40

b Kum 28:29

c Zb 107:27

SURA YA 13

d Ayu 23:3, 4
Ayu 31:35

e Ayu 16:2

f Met 17:28
Yak 1:19

Safu ya 2

a Zb 139:23
Yer 17:10

b Zb 50:20, 21
Yak 2:9

c Ayu 19:25
Zb 23:4

d Kut 15:2
Zb 27:1
Isa 12:2

e Ayu 27:8
Ayu 36:13
Isa 33:14

- 8** Je, mtamuunga mkono,*
Je, mtajaribu kumtetea Mungu wa kweli?
- 9** Je, mambo yatawaendea vyema akiwachunguza?^a
Je, mtamdanganya kama mnavyomdanganya mwanadamu anayeweza kufa?
- 10** Kwa hakika atawakemea Mkijaribu kwa siri kuonyesha upendeleo.^b
- 11** Je, adhama yake mwenyewe haitawaogopesha
Na hofu yake haitawaa-ngukia?
- 12** Misemo yenu ya hekima* ni methali za majivu;
Kujitetea kwenu* ni hafifu kama ngome za udongo.
- 13** Nyamazeni mbele yangu, ili niongee.
Kisha na yanipate yataka-yonipata!
- 14** Kwa nini ninajihatarisha*
Na kubeba uhai wangu* mikononi mwangu?
- 15** Hata akiniua, bado nita-ngoja;^c
Nitajitetea* mbele zake.
- 16** Ndipo atakapokuwa woku-vu wangu,^d
Kwa maana hakuna mtu aliyemkataa Mungu* anayeweza kuja mbele zake.^e
- 17** Sikilizeni kwa makini neno langu;
Sikilizeni tangazo langu.
- 18** Sasa tazameni, nimetayarisha kesi yangu;
Najua sina kosa.

13:8 *Au “mtampendelea.” 13:12 *Au “inayokumbukwa.” #Tnn., “Mafundo ya ngao zenu.” 13:14 *Tnn., “Kwa nini naubeba mwili wangu kwenye meno yangu?” #Au “nafsi yangu.” 13:15 *Au “Nitatetea njia zangu.” 13:16 *Au “mwasi imani.”

- 19** Ni nani atakayepambana nami?
Nitakufa, ikiwa nitanya-maza!*
- 20** Ee Mungu, nifanyie mambo mawili tu,*
Ili nisijifiche kutoka mbele zako:
- 21** Odoa mkono wako mzito uwe mbali nami,
Nawe usiache hofu yangu kukuelekea initishe.^a
- 22** Niite nami nitakujibu,
Au acha nizungumze, nawe unijibu.
- 23** Nimefanya makosa na dhambi gani?
Nifunulie kosa langu na dhambi yangu.
- 24** Kwa nini unauficha uso wako^b
Na kuniona kuwa adui yako?^c
- 25** Je, utajaribu kulitisha jani linalopeperushwa na upepo
Au kuyakimbiza majani makavu?
- 26** Kwa maana unaendelea kuandika mashtaka makali dhidi yangu,
Nawe unanifanya niwajibike kwa sababu ya dhambi nilizofanya nilipokuwa kijana.
- 27** Umeitia miguu yangu kati-ka mikatale,
Unavichunguza kwa maki-ni vijia vyangu vyote,
Nawe unafuata kila wayo wa mguu wangu.
- 28** Kwa hiyo mwanadamu*

13:19 *Au labda, "Ikiwa mtu anaweza kupambana nami, nitanyamaza na kufa." **13:20** *Tnn., "Mambo mawili tu, usinitende." **13:28** *Labda "mwanadamu" anayerejelewa ni Ayubu.

SURA YA 13

a Ayu 9:34, 35
Ayu 33:6, 7

b Zb 10:1
Zb 13:1
Zb 44:24

c Ayu 16:9
Ayu 19:11
Ayu 33:8-11

Safu ya 2

SURA YA 14

a Zb 39:5, 6
Yak 4:14

b Mwa 3:19
Mwa 47:9
Zb 90:10
Mhu 2:23

c Zb 103:15, 16
Isa 40:6
Yak 1:10, 11
1Pe 1:24

d 1Nya 29:15
Zb 102:11
Zb 144:4

e Zb 143:2

f Mwa 5:3
Zb 51:5
Ro 5:12

g Zb 39:4

h Zb 39:13

huoza kama kitu kili-chooza,
Kama vazi lililoliwa na nondo.*

- 14** "Mwanadamu anayeza-liwa na mwanamke,
Maisha yake ni mafupi^a na yamejaa taabu.*^b
- 2** Huchanua kama ua na kisha hunyauka;*^c
Hukimbia kama kivuli na kutoweka.^d
- 3** Naam, umemkazia jicho lako,
Nawe unamleta* mbele zako katika hukumu.^e
- 4** Ni nani anayeweza kutokeza mtu safi kutokana na mtu asiye safi?^f
Hakuna awezaye!
- 5** Ikiwa siku zake zinajulikana,
Basi unajua idadi ya miezi yake;
Umewekeka mpaka ambao hawezi kuvuka.^g
- 6** Yageuzie mbali macho yako ili apumzike,
Mpaka atakapomaliza siku yake, kama kibarua.^h
- 7** Kwa maana hata mti una tumaini.
Ukikatwa, utachipuka tena,
Na matawi yake yataendelea kukua.
- 8** Mizizi yake ikizeekea ardhini
Na kisiki chake kikifia udongoni,
- 9** Utachipuka unaponusa maji;
Nao utatokeza matawi kama mmea mpya.

13:28 *Aina fulani ya mdudu mharibifu. **14:1** *Au "msukosuko." **14:2** *Au labda, "hukatwa." **14:3** *Tnn., "unanileta."

- 10** Lakini mwanadamu hufa na kulala bila uwezo wowote;
Mwanadamu anapokufa, yuko wapi?^a
- 11** Maji hutoweka baharini, Na maji ya mto hupungua na kukauka.
- 12** Mwanadamu pia hulala naye haamki.^b
Mpaka mbingu zitakapokuwa hazipo tena, hawataamka,
Wala hawataamshwa kutoka katika usingizi wao.^c
- 13** Laiti ungenificha Kaburini,^{*d}
Ungenificha mpaka hasira yako ipite,
Laiti ungenipimia wakati hususa na kunikumbuka!^e
- 14** Mtu akifa, je, anaweza kuishi tena?^f
Nitangojea sikuzote za utumishi wangu wa kulazimishwa
Mpaka kitulizo changu kitakapokuja.^g
- 15** Utaita, nami nitakujibu.^h
Utaitamani sana* kazi ya mikono yako.
- 16** Lakini sasa, unaendelea kuhesabu kila hatua yangu;
Unatafuta tu dhambi zangu.
- 17** Kosa langu limefungiwa katika mfuko,
Nawe unaufunga uovu wangu kwa gundi.
- 18** Kama mlima unavyoanguka na kuporomoka
Na mwamba unavyong'oka mahali pake,

14:13 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 14:15 *Au "Utakuwa na hamu kubwa kwa ajili ya."

SURA YA 14

a Mhu 3:19, 20
Mhu 9:10

b Mhu 9:5
Mhu 12:5

c Zb 13:3
Yoh 11:11
Mdo 7:59, 60

d 1Sa 2:6
Isa 57:1, 2

e Lu 23:42
Yoh 5:28, 29
Ebr 11:35

f Yoh 11:25
Mdo 26:8
1Ko 15:12
Ufu 20:13

g Ayu 19:25

h Da 12:13
Yoh 5:28, 29
Yoh 11:43, 44

Safu ya 2

a Mhu 8:8
Isa 57:16

b Mhu 9:5, 6

SURA YA 15

c Ayu 2:11
Ayu 4:1

- 19** Kama maji yanavyomomonyoa mawe
Na mafuriko yanavyosomba udongo,
Ndivyo ulivyoharibu tumaini la mwanadamu anayeweza kufa.
- 20** Unaibadilea kumshinda nguvu mpaka anapoa-ngamia;^a
Unaibadili sura yake, na kumfukuza.
- 21** Wanawe wanaheshimiwa, lakini yeye hajui;
Wanadharauliwa, lakini yeye hatambui.^b
- 22** Huhisi maumivu anapokuwa tu angali hai;
Yeye* huomboleza wakati tu angali anaishi."

15 Elifazi^c Mtemani akajibu:

- 2** "Je, mtu mwenye hekima atajibu kwa hoja zisizo na maana,*
Au, je, atajaza tumbo lake upepo wa mashariki?"
- 3** Kukaripia kwa maneno matupu ni jambo lisilo na maana,
Na kuzungumza tu hakuna faida yoyote.
- 4** Kwa maana unafanya watu wasimwogope Mungu,
Na kuwazuia wasitafakari kamwe kumhusu Mungu.
- 5** Kwa maana kosa lako linakufanya useme unayosema,*
Nawe unachagua maneno ya hila.
- 6** Kinywa chako mwenyewe kinakuhukumu, wala si mimi;

14:22 *Au "Nafsi yake." 15:2 *Au "kwa ujuzi wa ubatili." 15:5 *Au "kosa lako linakiozea kinywa chako."

- Midomo yako mwenyewe inatoa ushahidi dhidi yako.^a
- 7 Je, wewe ndiye mwanadamu wa kwanza kuzaliwa, Au ulizaliwa kabla ya vilima?
- 8 Je, wewe husikiliza mazungumzo ya siri ya Mungu, Au ni wewe peke yako mwenye hekima?
- 9 Unajua nini ambacho sisi hatujui?^b
Unaelewa nini ambacho sisi hatuelewi?
- 10 Watu wenye mvi na wazee wako miongoni mwetu,^c
Watu wenye umri mkubwa kuliko baba yako.
- 11 Je, hutosheki na faraja za Mungu, Au maneno ya upole unayoambiwa?
- 12 Kwa nini moyo wako unakupeperusha, Na kwa nini macho yako yanawaka kwa hasira?
- 13 Kwa maana unaifanya roho yako imkasirikie Mungu, Nawe unaruhusu maneno ya aina hiyo yatoke kati-ka kinywa chako mwenyewe.
- 14 Mwanadamu anayeweza kufa ni nini hata awe safi, Au yeyote anayezaliwa na mwanamke ni nini hata awe mwadilifu?^d
- 15 Tazama! Hana imani na watakatifu wake, Na hata mbingu si safi machoni pake.^e
- 16 Sembuse mtu anayechukiza na aliyepotoka,^f

SURA YA 15

a Ayu 42:8

b Ayu 13:2
Ayu 16:2

c Ayu 32:6

d Ayu 25:4

e Ayu 25:5, 6
Ayu 42:7

f Ayu 4:18, 19

Safu ya 2

a Ayu 8:8

b Ayu 18:11
Ayu 20:25

c Ayu 18:12

Mwanadamu anayekunywa uovu kama maji!

- 17 Nitakujulisha; nisikilize! Nitasimulia mambo niliyoona,
- 18 Mambo ambayo watu wenyewe hekima wamejifunza kutoka kwa baba zao,^a
Mambo ambayo hawakuficha.
- 19 Ni wao peke yao waliopelewa nchi, Na hakuna mgeni aliyepita miongoni mwao.
- 20 Mtu mwovu huteseka siku zake zote, Miaka yote aliyotengewa mkandamizaji.
- 21 Masikio yake husikia sauti zenye kutisha;^b
Wakati wa amani, wavamizi humshambulia.
- 22 Haamini kwamba ataponyoka kutoka gizani;^c
Amekusudiwa kuuawa kwa upanga.
- 23 Hutangatanga akitafuta chakula*—kiko wapi? Anajua vizuri kwamba siku ya giza iko karibu.
- 24 Taabu na maumivu makali huendelea kumtisha; Humshinda nguvu kama mfalme aliye tayari kushambulia.
- 25 Kwa maana yeye huunyoo- sha mkono wake dhidi ya Mungu mwenyewe Na kujaribu kumpinga* Mweza-Yote;
- 26 Hukimbia kwa ukaidi kumshambulia Yeye, Akiwa na ngao yake nene, iliyo imara;*

15:23 *Tnn., "mkate." 15:25 *Au "kujaribu kumshinda." 15:26 *Tnn., "ngao yenye mafundo manene."

- 27** Uso wake umefunikwa kwa mafuta,
Na kiuno chake kimepanuka kwa mafuta;
- 28** Hukaa katika majiji yata-kayoangamizwa,
Katika nyumba ambazo hazitakaliwa na yeyote,
Ambazo zitakuwa marundo ya mawe.
- 29** Hatatajirika, na mali zake hazitaongezeka,
Wala vitu anavyomiliki havitaenea nchini.
- 30** Hatakimbia kutoka gizani; Mwali wa moto utakausha tawi lake,*
Naye atatoweka kwa kishindo cha pumzi ya kinywa cha Mungu.^{#a}
- 31** Hapaswi kukengeushwa na kutumaini mambo yasiyo na thamani,
Kwa sababu atakachopata badala yake hakitakuwa na thamani;
- 32** Hilo litatendeka kabla ya siku yake,
Na matawi yake hayatasi-tawi kamwe.^b
- 33** Atakuwa kama mzabibu unaoangusha zabibu zake mbichi,
Na kama mzeituni unaoangusha maua yake.
- 34** Kwa maana kusanyiko la watu wanaomkataa Mungu* ni tasa,^c
Na moto utateketeza mahema ya rushwa.
- 35** Wanatunga mimba ya matatizo na kuzaa uovu,
Na tumbo lao la uzazi huzaa udanganyifu.”

15:30 *Yaani, tumaini lolote la kupona. ^{#Tnn.}, “chake.” 15:34 *Au “waasi imani.”

SURA YA 15

a Ayu 4:9

b Ayu 22:15, 16

c Ayu 8:11-13

Safu ya 2

SURA YA 16

a Ayu 13:4, 5
Ayu 19:2, 3b Zb 109:25
Mt 27:39c Met 27:9
Mt 7:12
Ro 12:15
1Pe 3:8

d Ayu 2:13

e Ayu 7:3

f Ayu 10:16

16 Ayubu akajibu:
2 “Nimeshasikia mambo mengi kama hayo.

Ninyi nyote ni wafariji wasumbufu!^a

3 Je, maneno yasiyo na maana* yana mwisho? Ni nini kinachowachochea kujibu hivi?

4 Mimi pia ningeweza kuzungumza kama ninyi. Ikiwa mngekuwa katika hali yangu,*

Ningetoa hoja zenye kusa-dikisha dhidi yenu Na kuwatikisia kichwa changu.^b

5 Hata hivyo, badala yake, ningewaimarisha kwa maneno ya kinywa changu,

Na faraja ya midomo yangu ingewatuliza.^c

6 Nikiingea, maumivu yangu mwenyewe hayatulii,^d

Nami nikiacha kuongea, maumivu yangu yanapungua kwa kadiri gani?

7 Lakini sasa amenichosha;^e Ameiangamiza nyumba yangu yote.*

8 Pia unanikamata, na wengine wameshuhudia jambo hilo,

Hivi kwamba kukonda kwangu kumezidi na kunatoa ushahidi mbele yangu.

9 Hasira yake imenirarua vipandevipande, naye ana chuki kunielekea.^f

16:3 *Au “ya ubatili.” 16:4 *Au “Ikiwa nafsi zenu zingechukua nafasi ya nafsi yangu.” 16:7 *Au “Amewaangamiza wale wanaokusanyika nami.”

- Hunisagia meno yake.
Adui yangu hunitoboa kwa macho yake.^a
- 10** Wamefumbua vinywa vyao wazi dhidi yangu,^b
Nao wameyapiga mashavu yangu kwa dharau;
Wanakusanyika kwa wingi dhidi yangu.^c
- 11** Mungu hunitia mikononi mwa wavulana,
Naye hunitupa kwa nguvu mikononi mwa waovu.^d
- 12** Nilikuwa na amani, lakini akanivunjavunja;^e
Alinikamata nyuma shingoni na kunipondaponda;
Kisha akanifanya shabaha yake.
- 13** Wapiga mishale wake wananizunguka;^f
Huzichoma figo^g zangu bila huruma;
Humwaga nyongo yangu ardhini.
- 14** Hunitoboa tena na tena kama ukuta;
Hunishambulia kama shujaa.
- 15** Nimeshona nguo ya magunia ili kufunika ngozi yangu,^h
Nami nimezika heshima yangu* mavumbini.ⁱ
- 16** Uso wangu ni mwekundu kwa sababu ya kulia,^j
Na kuna kivuli kizito* juu ya kope zangu,
- 17** Ingawa mikonu yangu haijatenda ukatili wowote
Na sala yangu ni safi.
- 18** Ee dunia, usiifunike damu yangu!^k

16:15 *Au "nguvu zangu." Tnn., "pembe yangu." 16:16 *Au "kivuli cha kifo."

SURA YA 16

a Ayu 33:8-10

b Zb 22:13

c Zb 35:15

d Zb 27:12

e Ayu 1:12, 17

f Ayu 7:20

g Zb 73:21

h 1Fa 21:27
2Fa 6:30i Ayu 30:19
Zb 7:5j Zb 6:6
Zb 31:9
Omb 1:16k Mwa 4:8, 10
Zb 72:14

Safu ya 2

a Ayu 12:4

b Zb 40:1
Zb 142:2

c Ayu 31:35

d Ayu 7:9
Ayu 14:10
Mhu 12:5

SURA YA 17

e Zb 88:3, 4
Isa 38:10f Zb 35:16
Ebr 11:36

g Met 17:18

h 2Sa 17:14
Isa 6:10
Mt 11:25

Acha kilio changu
kisiwe na mahali pa
kupumzikia!

- 19** Hata sasa, shahidi wangu yuko mbinguni;
Yule anayeweza kunitetea yuko juu.
- 20** Rafiki zangu wananidhihaki^a
Huku macho yangu yakimwaga machozi* nikimlilia Mungu.^b
- 21** Acha mtu fulani awe mwamuzi kati ya mwana-damu na Mungu,
Kama anavyoweza kuwa mwamuzi kati ya mtu mmoja na mwenzake.^c
- 22** Kwa maana miaka iliyobaki ni michache,
Nami nitafuata njia ambayo wale wanaoifuata hawarudi.^d

17 "Roho yangu imevunjwa, siku zangu zimezimwa;

Makaburi yananingojea.^e

2 Wadhihaki wananizunguka,^f

Na macho yangu yanalizimika kutazama* uasi wao.

3 Tafadhali ikubali dhama-na yangu, na ukae nayo.

Ni nani mwingine atakayenipa mkono wake na kutoa dhama-na kwa nia-ba yangu?^g

4 Kwa sababu umeficha utambuzi mbali na moyo wao;^h

Ndiyo maana huwakwezi.

5 Huenda akajitolea kushiriki vitu vyake na rafiki zake,

16:20 *Au labda, "yakikosa usingizi." 17:2 *Au "kuendelea kuangalia."

Huku macho ya watoto wake yakidhoofika.

- 6** Amenifanya niwe kitu cha kudharauliwa* miongoni mwa mataifa,^a

Hivi kwamba nikawa mtu wanayemtemea mate usoni.^b

- 7** Macho yangu yanafifia kwa sababu ya maumivu makali,^c

Na viungo vyangu vyote ni kivuli tu.

- 8** Watu wanyoofu wananitazama kwa mshangao, Na asiye na hatia anasumbuka kwa sababu ya mtu anayemkataa Mungu.*

- 9** Mwadilifu anaendelea ku-shikamana na njia yake,^d Na mwenye mikono safi anazidi kuwa na nguvu.^e

- 10** Hata hivyo, nyote mna-weza kuja na kuendelea kunishambulia kwa hoja zenu,

Kwa maana sijamwona yeyote mwenye hekima miongoni mwenu.^f

- 11** Siku zangu zimekwisha;^g Mipango yangu, tamaa za moyo wangu, zimevunjwawunjwa.^h

- 12** Wanaendelea kufanya usiku uwe mchana, Wakisema, 'Bila shaka mwangaza unakaribia kwa sababu kuna giza.'

- 13** Nikisubiri, Kaburi* litakuwa makao yangu;ⁱ Nitakitandaza kitanda changu gizani.^j

17:6 *Tnn., "methali; msemu." 17:8 *Au "mwasi imani." 17:13, 16 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 17

a Zb 69:11, 12

b Ayu 30:9, 10

c Ayu 16:16
Zb 6:7
Zb 31:9

d Zb 119:165

e Zb 24:3, 4
Zb 84:5, 7

f Ayu 6:29

g Ayu 7:6
Ayu 9:25
Isa 38:10

h Yak 4:13, 14

i Mhu 12:5, 7

j Ayu 10:21, 22

Safu ya 2

a Zb 49:7, 9
Zb 143:7

b Ayu 7:6
Ayu 14:19
Ayu 19:10

c Mwa 3:19
Ayu 3:19

SURA YA 18

d Ayu 2:11
Ayu 8:1

e Zb 73:22

f Ayu 8:13, 14
Ayu 11:20

g Ayu 5:13

- 14** Nitaliambia shimo**^a kwa sauti, 'Wewe ni baba yangu!'

Na mabuu, 'Ninyi ni mama yangu na dada yangu!'

- 15** Basi, tumaini langu liko wapi?^b

Ni nani anayeweza kuona tumaini hilo?

- 16** Litashuka[#] kwenye malango ya Kaburi* yenye makomeo

Tutakaposhuka sote pamoja mavumbini."^c

18 Bildadi^d Mshua akajibu:

- 2** "Utaendelea kusema maneno haya mpaka lini? Onyesha uelewaji kidogo ili nasi tuseme.

- 3** Kwa nini tuonwe kama wanyama^e

Na kuonekana wapumbavu* machoni pako?

- 4** Hata ukijirarua* vipandevipande kwa hasira, Je, dunia itaachwa kwa ajili yako,

Au mwamba kuhama mahali pake?

- 5** Naam, nuru ya mwovu itazimwa, Na mwali wa moto wake hautang'aa.^f

- 6** Hakika nuru iliyo ndani ya hema lake itakuwa giza, Na taa iliyo juu yake itazimwa.

- 7** Hatua zenye nguvu zimefupishwa, Na shauri lake mwenyewe litamwangusha.^g

- 8** Kwa maana miguu yake itamwongoza kwenye wavu,

17:14 *Au "kaburi." 17:16 #Yaani, tumaini langu. 18:3 *Au labda, "wasio safi." 18:4 *Au "ukiirarua nafsi yako."

Naye atangatanga kwenye kamba za wavu.

- 9** Mtego utamnasa kisigino; Na kitanzi kitamkamata.^a
- 10** Kamba imefichwa ardhini kwa ajili yake, Na mtego uko kwenye kijia chake.
- 11** Vitisho vinamwogopesha pande zote^b Na kumfuatia miguuni pake.
- 12** Nguvu zake zimepungua, Na msiba^c utamfanya ayu-mbeyumbe.*
- 13** Ngozi yake imeliwa; Ugonjwa hatari sana unakula* viungo vyake.
- 14** Ameng'olewa kutoka katika hema lake lililo salama^d Na kupelekwa kwa mfalme wa vitisho.*
- 15** Wageni watakaa* katika hema lake; Kiberiti kitatawanywa juu ya makao yake.^e
- 16** Chini yake, mizizi yake itakauka, Na juu yake, matawi yake yatanyauka.
- 17** Hakuna atakayemkumbuka duniani, Na jina lake halitajulikana* mtaani.
- 18** Ataondolewa kwenye nuru na kupelekwa gizani Na kufukuzwa kutoka duniani.*
- 19** Hatakuwa na mtoto wala mzao miongoni mwa watu wake,

18:12 *Au "achechemee." 18:13 *Tnn., "Mzaliwa wa kwanza wa kifo anakula." 18:14 *Au "kifo kinachotisha." 18:15 *Tnn., "Kitu ambacho si chake kitakaa." 18:17 *Tnn., "hatakuwa na jina." 18:18 *Au "kwenye ardhini inayozaa."

SURA YA 18

a Ayu 5:5
Ayu 22:5,10

b Ayu 15:21
Ayu 20:25

c Ayu 15:23

d Ayu 11:20

e Kum 29:22, 23

Safu ya 2

SURA YA 19

a Zb 42:10

b Zb 55:21
Met 12:18

c Met 18:24

d Zb 22:2
Hab 1:2

e Lu 18:7

f Ayu 3:23
Zb 88:8

Wala hakuna atakayebaki katika makao yake.*

- 20** Siku yake itakapofika, watu wa Magharibi wata-shituka sana Na watu wa Mashariki watashikwa na hofu.
- 21** Hivyo ndivyo inavyokuwa Na kwa makao ya mtu ambaye hajamjua Mungu."

19 Ayubu akajibu:

- 2** "Mtaendelea kunika-sirisha* mpaka lini,^a Na kuniponda kwa maneno?^b
- 3** Mmenikemea* mara kumi sasa; Mnanitesa bila aibu.^c
- 4** Na ikiwa kwa kweli nilifanya kosa, Ni kosa langu mimi mwenyewe.
- 5** Ikiwa mnasisitiza kujikweza juu yangu, Mkidai kwamba mna haki ya kunishutumumu,
- 6** Basi, jueni kwamba Mungu ndiye ameni-potosha, Naye ameninasa katika wavu wake wa kuwindia.
- 7** Tazameni! Naendelea kulia kwa sauti, 'Ukatili!' lakini sijibiwi;^d Naendelea kulilia msaada, lakini hakuna haki.^e
- 8** Ameziba kijia changu kwa ukuta wa mawe, siwezi kupita; Amezifunika njia zangu kwa giza.^f

18:19 *Au "makao yake ya muda." 19:2 *Au "kuikasarisha nafsi yangu." Angalia Kamusi, uku. 2012. 19:3 *Au "Mmenitukana."

- 9 Amenivua utukufu wangu
Na kunivua taji kichwani.
- 10 Hunibomoa kila upande
na kuniangamiza;
Anang'oa tumaini langu
kama mti.
- 11 Hasira yake huwaka dhidi
yangu,
Naye huniona kuwa adui
yake.^a
- 12 Majeshi yake hukusanyika
na kunizingira,
Nayo hupiga kambi kuzu-
nguka hema langu.
- 13 Ndugu zangu wenyewe
amewafukuza mbali
nami,
Na wale wanaonijua wame-
geuka na kuniacha.^b
- 14 Rafiki zangu wa karibu*
wametoweka,
Na wale niliowajua vema
wamenisahau.^c
- 15 Wageni walio nyumbani
mwangu^d na vijakazi
wangu wananiona kuwa
mgeni;
Mimi ni mgeni machoni
pao.
- 16 Ninamwita mtumishi
wangu, lakini hajibu;
Namsihi kwa kinywa
changu anihurumie.
- 17 Pumzi yangu mwenyewe
inamchukiza mke
wangu,^e
Nami ni uvundo kwa
ndugu* zangu wenyewe.
- 18 Hata watoto wachanga
wananidharau;
Ninaposimama, wanaanza
kunifanyia mzaha.
- 19 Rafiki zangu wote wa kari-
bu wananichukia,^f

19:14 *Au "Watu wangu wa ukoo."
19:17 *Tnn., "wana wa tumbo langu la
uzazi," yaani, tumbo lililonibeba (tumbo
la mama yangu).

SURA YA 19

a Ayu 13:24

b Zb 31:11
Zb 69:8

c Zb 38:11

d Ayu 31:32

e Ayu 2:9

f Ayu 17:6
Zb 88:8

Safu ya 2

a Zb 109:5

b Ayu 30:30
Zb 102:5c Ayu 1:10-12
Zb 38:2

d Ayu 2:9,10

e Zb 69:26

f Ayu 14:14
Zb 19:14
Zb 69:18
Zb 103:2,4
Mt 20:28
Mk 10:45

g Zb 17:15

h Zb 69:26

Na wale niliowapenda
wamenigeuka.^a

- 20 Mifupa yangu inashikama-
na na ngozi yangu na
mwili wangu,^b
Nami ninaponyoka kwa
ngozi ya meno yangu.
- 21 Nionyesheni rehema, ra-
fiki zangu, nionyesheni
rehema,
Kwa maana mkono wa
Mungu mwenyewe ume-
nigusa.^c
- 22 Kwa nini mnaendelea
kunitesa kama Mungu
anavyonitesa,^d
Mkinishambulia bila
kuacha?^{*e}
- 23 Laiti maneno yangu
yangeandikwa,
Laiti yangeandikwa katika
kitabu!
- 24 Laiti yangechongwa mile-
le kwenye mwamba,
Kwa kalamu ya chuma na
risasi!
- 25 Kwa maana najua vizuri
kwamba mkombozi
wangu^f yuko hai;
Atakuja baadaye na kuinu-
ka juu ya dunia.*
- 26 Baada ya ngozi yangu
kuharibiwa hivi,
Nikiwa bado hai, nitamwo-
na Mungu,
- 27 Ambaye mimi mwenyewe
nitamwona,
Ambaye macho yangu
mwenyewe yatamwona,
si ya mwingine.^g
Lakini ndani kabisa nina-
hisi nimelemewa!^{*}
- 28 Kwa maana mnauliza, "Tu-
namtesa kwa njia gani?"^h

19:22 *Tnn., "Na hamtosheki na mwili
wangu?" 19:25 *Tnn., "juu ya (kwenye)
mavumbi." 19:27 *Au "Figo zangu zi-
meacha kufanya kazi."

Kwa maana mimi ndiye
mzizi wa tatizo hili.

29 Ninyi wenyewe ogopeni
upanga,^a

Kwa kuwa upanga huwaa-
dhibu wakosaji;
Mnapaswa kujua kwamba
kuna mwamuzi.”^b

20 Sofari^c Mnaamathi
akajibu:

2 “Ndiyo sababu mawazo
yangu mwenyewe yana-
yonifadhaisha
yananichochea kujibu
Kwa sababu ya mahangai-
ko niliyo nayo.

3 Nimesikia karipio linaloni-
vunjia heshima;
Na uelewaji wangu unani-
chochea* kujibu.

4 Bila shaka unajua jambo
hili tangu zamani,
Kwa maana imekuwa
hivyo tangu mtu*
alipoumbwa duniani,^d

5 Kwamba kelele za sha-
ngwe za mwovu ni za
muda mfupi
Na kushangilia kwa mtu
anayemkataa Mungu* ni
kwa kipindi kifupi.^e

6 Ingawa ukuu wake hupa-
nda mpaka mbinguni
Na kichwa chake hufika
mawinguni,

7 Ataangamia milele kama
kinyesi chake mwe-
nyewe;
Wale waliozoea kumwona
watauliza, ‘Yuko wapi?’

8 Atatoweka kama ndoto,
nao hawatampata;
Atafukuzwa mbali kama
maono ya usiku.

20:3 *Tnn., “roho inayotoka katika
uelewaji wangu inanichochea.” 20:4
*Au “mwanadamu; Adamu.” 20:5 *Au
“mwasi imani.”

SURA YA 19

a Kum 32:41

b Zb 58:11
Mt 7:1
Ro 14:4
Yak 4:12

SURA YA 20

c Ayu 2:11
Ayu 11:1

d Ayu 8:8

e Ayu 8:13, 19
Ayu 21:28

Safu ya 2
a Ayu 8:13, 18

b Ayu 20:18

c Ayu 20:10

9 Jicho lililomwona halita-
mwona tena,
Na mahali pake hapata-
mwona tena.^a

10 Watoto wake mwenyewe
watawaomba maskini
msaada,
Na mikono yake mwe-
nyewe itarudisha mali
aliyochukua.^b

11 Mifupa yake ilijaa nguvu
za ujana,

Lakini nguvu hizo zitalala
pamoja naye mavumbini.

12 Ikiwa uovu ni mtamu
kinywani mwake,
Ikiwa anauficha chini ya
ulimi wake,

13 Ikiwa anauonja na hau-
temi
Lakini anauacha ukae
kinywani mwake,

14 Chakula chake kitageuka
na kuwa kichungu ndani
yake;
Kitakuwa kama sumu* ya
swila ndani yake.

15 Amemeza mali, lakini
ataitapika;
Mungu ataitoa yote
tumboni mwake.

16 Atanyonya sumu ya swila;
Meno ya nyoka kipiri yata-
muua.*

17 Hataona kamwe vijito vya
maji,
Mafuriko ya asali na siagi.

18 Atarudisha mali zake bila
kuzitumia;*
Hatafurahia utajiri wa
biashara yake.^c

19 Kwa maana amewaconda
na kuwaacha maskini;
Amenyakua nyumba
ambayo hakujenga.

20:14 *Au “nyongo.” 20:16 *Tnn., “Uli-
mi wa nyoka kipiri utamuua.” 20:18
*Tnn., “naye hatameza.”

- 20** Lakini hatakuwa na amani ndani yake;
Mali zake hazitamsaidia kuokoka.
- 21** Hakuna chochote kina-chobaki cha kunyafua;
Ndiyo sababu ufanisi wake hautadumu.
- 22** Mali zake zitakapofikia kilele, mahangaiko yata-mkumba;
Misiba itamshambulia kwa nguvu zote.
- 23** Atakapokuwa akijaza tumbo lake,
Mungu atammwagia hasira yake kali,
Itamnyeshea mpaka ndani ya matumbo yake.
- 24** Atakapokimbia silaha za chuma,
Mishale kutoka katika upinde wa shaba itamchoma.
- 25** Huchomoa mshale mgongoni mwake,
Silaha inayong'aa kutoka kwenye nyongo yake,
Naye hushikwa na hofu.^a
- 26** Giza zito linasubiri hazina zake;
Moto ambao haukuwa-shwa na yeyote utamla;
Msiba unamsubiri yeyote atakayeokoka katika hema lake.
- 27** Mbingu zitafunua kosa lake;
Dunia itainuka dhidi yake.
- 28** Mafuriko yataifagilia mba-li nyumba yake;
Yatakuwa mafuriko yenye nguvu katika siku ya hasira ya Mungu.
- 29** Hilo ndilo fungu ambalo Mungu atampa mwovu,
Urithi ambao Mungu amemtangazia.”

SURA YA 20

a Ayu 15:21
Ayu 18:5,11

Safu ya 2

SURA YA 21

a Ayu 16:10,20
Ayu 17:2
Ebr 11:36

b Hab 1:3,13

c Ayu 12:6
Zb 37:7
Zb 73:3
Zb 73:12
Yer 12:1

d Zb 73:3,5

- 21** Ayubu akajibu:
- 2** “Sikilizeni kwa maki-ni ninayosema;
Na hii iwe faraja mnayo-nipa.
- 3** Nivumilieni ninapozungu-mza;
Nikimaliza kuzungumza, mnaweza kunidhihaki.^a
- 4** Je, ninamlalamikia mwa-nadamu?
Ikiwa ndivyo, je, nisinge-kosa* subira?
- 5** Niangalieni na kuniko-dolea macho kwa mshangao;
Funikeni kinywa chenu kwa mkono wenu.
- 6** Ninapofikiria jambo hilo, nashikwa na wasiwasi,
Na mwili wangu wote una-tetemeka.
- 7** Kwa nini waovu wanae-ndelea kuishi,^b
Wanazeeka, na kutaji-rika? *^c
- 8** Huwaona watoto wao sikuzote,
Nao huendelea kuishi na kuwaona wazao wao.
- 9** Nyumba zao zina usa-lama, hawana hofu yoyote,^d
Na Mungu hawaadhibu kwa fimbo yake.
- 10** Ng'ombe dume wao hawa-shindwi kuzalisha;
Ng'ombe wao huzaa na mimba haziharibiki.
- 11** Wavulana wao hukimbia nje kama kondoo,
Na watoto wao hurukaru-ka huku na huku.
- 12** Wao huimba kwa tari na kinubi

21:4 *Tnn., “roho yangu isingekosa.”

21:7 *Au “kuwa na nguvu.”

- Na kushangilia wanaposi-
kia sauti ya zumari.*^a
- 13** Huishi siku zao wakiwa
wameridhika
Nao hushuka kwa amani*
Kaburini.*^f
- 14** Lakini wanamwambia Mu-
ngu wa kweli, "Tuache!
Hatutamani kuzijua njia
zako.*^b
- 15** Mweza-Yote ni nani ili
tumtumikie?c
Tutapata faida gani tuki-
mfahamu?d
- 16** Lakini ninajua kwamba
hawaudhibiti ufanisi
wao wenyewe.e
Mawazo ya waovu yako
mbali nami.*^f
- 17** Ni mara ngapi taa ya
waovu huzimwa?g
Ni mara ngapi wanapopa-
twa na msiba?
Ni mara ngapi Mungu hu-
waangamiza kwa hasira
yake?
- 18** Je, kuna wakati wowote
wanapopeperushwa na
upepo kama majani
makavu
Na kama makapi yana-
yopeperushwa mbali na
upepo wa dhoruba?
- 19** Mungu atawawekea wato-
to wa mtu mwovu
adhabu ya mtu huyo.
Lakini Mungu na amlipe ili
apate kujua hilo.h
- 20** Macho yake mwenyewe na
yaone maangamizi yake,
Na anywe mwenyewe gha-
dhabu ya Mweza-Yote.i

21:12 *Au "filimbi." **21:13** *Au "ha-
raka," yaani, wanakufa upesi bila mau-
mivu. ^aAu "Sheoli." Angalia Kamusi,
uku. 2012. **21:16** *Au "Mashauri; Nja-
ma za waovu ziko mbali nami."

SURA YA 21

a Isa 5:12
Isa 22:13
Amo 6:4, 5

b Zb 10:4, 11
Zb 73:3, 11

c Kut 5:2
Zb 10:4
Ho 13:6

d Mal 3:14

e Lu 12:19, 20

f Zb 1:1

g Met 13:9
Met 20:20
Met 24:20

h Zb 11:6
Isa 26:11

i Zb 75:8
Isa 51:17
Yer 25:15
Ufu 14:10

Safu ya 2

a Zb 55:23

b Isa 40:13, 14
Ro 11:34
1Ko 2:16

c Isa 40:23

d Zb 49:17
Lu 12:19, 20

e Zb 73:12, 19
Mt 24:38, 39

f Ayu 3:19
Mhu 9:2

g Ayu 24:20

h Zb 59:3

i Ayu 20:5, 7

- 21** Kwa maana, kwa nini aha-
ngaikie kitakachoipata
nyumba yake baada ya
kifo chake
Ikiwa idadi ya miezi yake
imepunguzwa?*^a
- 22** Je, kuna yeyote anayewe-
za kumfundisha Mungu
ujuzi,*^b
Wakati Yeye ndiye ana-
yewahukumu hata walio
juu zaidi?c
- 23** Kuna mtu anayekufa aki-
wa na nguvu zake zote^d
Akiwa amestarehe kabisa
na bila mahangaia,e
- 24** Wakati mapaja yake yame-
nenepa kwa mafuta
Na mifupa yake ikiwa na
nguvu.*
- 25** Lakini mtu mwingine hufa
akiwa ametaabika sana,*
Akiwa hajaonja kamwe
vitu vyema.
- 26** Wote watalala mavu-
mbini,f
Na mabuu yatawafunika
wote wawili.g
- 27** Tazama! Ninajua vizuri
mambo mnayofikiria
Na njama mnazopanga ili
kunidhuru.*^h
- 28** Kwa maana mnasema,
'Iko wapi nyumba ya yule
mtu maarufu,
Na liko wapi hema alimoi-
shi yule mtu mwovu?i
- 29** Je, hamjawauliza wasa-
firi?
Je, hamchunguzi kwa ma-
kini mambo waliyoona,*

21:21 *Au "imegawanywa mara mbi-
li." **21:22** *Au "kumfundisha Mungu ja-
mbo lolote." **21:24** *Tnn., "umajimaji
ulio mifupani haujakauka." **21:25** *Au
"akiwa na uchungu nafsini." **21:27** *Au
labda, "ili kunitendea kikatili." **21:29**
*Tnn., "ishara zao."

- 30** Kwamba mtu mwovu huokolewa katika siku ya msiba
Na kuokolewa katika siku ya ghadhabu?
- 31** Ni nani atakayemuuliza kuhusu njia yake,
Na ni nani atakayemlipa kwa sababu ya mambo aliyotenda?
- 32** Anapopelekwa kaburini, Kaburi lake litalindwa.
- 33** Mabonge ya udongo wa bondeni* yatakuwa matamu kwake,^a
Na wanadamu wote humfuata^{#b}
Kama idadi isiyohesabika ya waliomtangulia.
- 34** Basi kwa nini mnipe faraja isiyo na maana?^c
Majibu yenu hayana lolote isipokuwa udanganyifu!”
- 22** Elifazi^d Mtemani aka-jibu:
- 2** “Je, mwanadamu anaweza kuwa na faida kwa Mungu?
Je, mtu yeyote mwenye ufahamu anaweza kuwa na faida kwake?^e
- 3** Je, Mweza-Yote anajali* kwamba wewe ni mwadilifu,
Au je, anapata faida yoyote kwa sababu unafuata njia ya utimilifu?^f
- 4** Je, atakuadhibu Na kukushtaki kwa sababu unamheshimu?
- 5** Je, si kwa sababu uovu wako mwenyewe ni mku-bwa sana
Na makosa yako hayana mwisho?^g

21:33 *Au “korongoni.” #Tnn., “Naye atawakokota wanadamu wote wamfuata.” 22:3 *Au “anafurahi.”

SURA YA 21

a Ayu 3:17

b Ro 5:12

c Ayu 16:2, 3

SURA YA 22

d Ayu 2:11

Ayu 4:1

e Ayu 15:14, 15

f Ayu 2:3

Ayu 32:3

g Ayu 1:8

Ayu 4:7

Safu ya 2

a Ayu 31:19, 22

b Ayu 31:17, 22

c Ayu 31:25, 28

d Ayu 18:5, 9

- 6** Kwa maana unachukua dhamana kutoka kwa ndugu zako bila sababu, Nawe unawavua watu mavazi yao na kuwaacha uchi.*^a
- 7** Humpi aliyechoka maji ya kunywa,
Nawe unamnyima chakula mwenye njaa.^b
- 8** Nchi ni ya mtu mwenye nguvu,^c
Na anayependelewa huishi ndani yake.
- 9** Lakini uliwafukuza wajane mikono mitupu,
Nawe uliiponda mikono ya mayatima.
- 10** Ndiyo sababu umezungu-kwa na mitego,*^d
Na vitisho vya ghafla vina-kuogopesha;
- 11** Ndiyo sababu kuna giza sana hivi kwamba huwezi kuona,
Na mafuriko ya maji yamekufunika.
- 12** Je, Mungu hayuko katika vilele vya mbinguni?
Na tazama jinsi nyota zote zilivyo juu sana.
- 13** Lakini umesema: ‘Kwa kweli Mungu anajua nini?
Je, anaweza kuhukumu katika giza zito?’
- 14** Mawingu humfunika hivi kwamba haoni
Anapotembea huku na kule kwenye duara ya mbingu.’
- 15** Je, utafuata kijia cha kale Ambacho watu waovu wamefuata,

22:6 *Tnn., “unawavua walio uchi mavazi yao.” 22:10 *Tnn., “mitego ya ndege.”

- 16** Watu ambao waliangami-
zwa* kabla ya wakati
wao,
Ambao msingi wao ulifagi-
liwa na mafuriko?#^a
- 17** Walikuwa wakimwambia
Mungu wa kweli: ‘Achana
nasi!’
Na ‘Mweza-Yote anaweza
kutufanya nini?’
- 18** Lakini, Yeye ndiye aliye-
zijaza nyumba zao vitu
vizuri.
(Sina mawazo maovu
kama hayo.)
- 19** Waadilifu wataona hilo na
kushangilia,
Na wasio na hatia watawa-
dhihaki na kusema:
- 20** ‘Wapinzani wetu wamea-
ngamizwa,
Na moto utateketeza
mabaki yao.’
- 21** Mjue Yeye, nawe utakuwa
na amani;
Kisha mambo mema yata-
kujia.
- 22** Kubali sheria inayotoka
katika kinywa chake,
Na uyaweke maneno yake
moyoni mwako.^b
- 23** Ukimrudia Mweza-Yote,
utarudishiwa hali
njema;^c
Ukiondoa uovu katika
hema lako,
- 24** Ukitupa dhahabu yako*
mavumbini
Na dhahabu ya Ofiri^d
kwenye miamba ya
mabondeni,[#]
- 25** Ndipo Mweza-Yote ataka-
pokuwa dhahabu yako,*

22:16 *Au “ambao maisha yao yalifupishwa.” #Tnn., “mto.” 22:24 *Au “Ukitupa vipande vyako vya dhahabu.” #Au “makorongoni.” 22:25 *Au “vipande vyako vya dhahabu.”

SURA YA 22

a Ayu 4:18,19

b Ayu 11:13

c Ayu 8:5,6

d 1Fa 9:28
Ayu 28:16
Zb 45:9
Isa 13:12

Safu ya 2

SURA YA 23

a Ayu 10:1

b Ayu 13:3
Ayu 16:21

c Ayu 31:37

- Naye atakuwa fedha yako
iliyo bora kabisa.
- 26** Kwa maana ndipo uta-
kapopendezwa na
Mweza-Yote,
Nawe utauinua uso wako
kumwelekea Mungu.
- 27** Utamsihi, naye atakusiki-
liza;
Nawe utatimiza nadhiri
zako.
- 28** Jambo lolote utakalo-
amua kufanya
litafanikiwa,
Na nuru itaangaza kwenye
kijia chako.
- 29** Kwa maana utaaibishwa
ukiongea kwa kiburi,
Lakini atawaokoa wanye-
nyekevu.*
- 30** Atawaokoa watu wasio na
hatia;
Kwa hiyo ikiwa mikono
yako ni safi, hakika
utaokolewa.”
- 23** Ayubu akajibu:
2 “Hata leo nitalalami-
ka kwa ukaidi;#^a
Nimeishiwa na nguvu kwa
sababu ya kulia kwa
uchungu.
- 3** Laiti ningejua mahali
ninapoweza kumpata
Mungu!^b
Ningeenda mahali
anapoishi.^c
- 4** Ningepeleka kesi yangu
mbele zake
Na kujaza hoja za kujitetea
kinywani mwangu;
- 5** Ningefahamu jinsi amba-
vyo angenijibu
Na kutilia maanani anayo-
niambia.

22:29 *Au “walio na macho yanayotazama chini.” 23:2 *Au “lalamiko langu ni uasi.”

- 6** Je, angepambana nami kwa nguvu zake nyingi? Hapana, bila shaka angeni-sikiliza.^a
- 7** Huko mtu mnyoofu ange-nyoosha mambo pamoja naye, Na Mwamuzi wangu angefutulia mbali mashtaka yangu milele.
- 8** Lakini nikienda mashariki, hayuko huko; Na nikirudi, simpati.
- 9** Anapofanya kazi upande wa kushoto, siwezi kumwona; Kisha anageuka upande wa kulia, lakini bado simwoni.
- 10** Lakini anajua kijia nina-chofuata.^b Baada ya kunijaribu, nitatoka nikiwa kama dhahabu safi.^c
- 11** Miguu yangu imefuata nyayo zake kwa ukaribu; Nimefuata njia yake bila kukengeuka.^d
- 12** Sijaacha amri ya midomo yake. Nimeyathamini maneno yake^e kama hazina hata kuliko nilivyoamriwa.*
- 13** Anapokusudia, ni nani anayeweza kumpinga?^f Anapotaka kufanya jambo, yeye hulifanya.^g
- 14** Kwa maana atatenda kwa ukamili aliyokusudia* kwa ajili yangu, Naye ana mambo mengi kama hayo akibani.
- 15** Ndiyo sababu nina wasi-wasi kwa sababu yake; Ninapomfikiria, hofu yangu inaongezeka.

23:12 *Au "nilivyoagizwa." 23:14 *Au "aliyoagiza."

SURA YA 23

a Zb 22:24
Isa 57:16

b Ayu 1:8
Zb 1:6
Zb 139:1

c Ayu 31:6
Zb 17:3

d Zb 18:21
Zb 44:18

e Zb 119:11, 127
Yer 15:16

f Ro 9:19

g Hes 23:19
Zb 135:6
Isa 14:24
Isa 46:10

Safu ya 2

SURA YA 24

a Hab 1:2

b Kum 19:14
Kum 27:17
Met 23:10
Ho 5:10

c Kum 24:17

d Zb 109:16
Met 22:16
Isa 10:1, 2
Yak 5:4

e Isa 32:14
Yer 14:6

f Kut 22:26, 27
Kum 24:13

16 Mungu amenifanya nihofu, Na Mweza-Yote amenitia woga.

17 Lakini bado sijanyamazi-shwa na giza Wala utusitisi uliofunika uso wangu.

24 "Kwa nini Mweza-Yote haweki wakati wa hukumu?"^a

Kwa nini wale wanaomjua hawaioni siku yake?*

2 Watu husogeza alama za mipaka;^b

Wanaiba mifugo kwa ajili ya malisho yao.

3 Huwachukua punda wa mayatima

Na kumchukua ng'ombe dume wa mjane kuwa dhamana ya mkopo.*^c

4 Huwasukuma maskini waondoke barabarani;

Watu wasio na uwezo duniani hulazimika kuji-ficha kwa sababu yao.^d

5 Maskini hutafuta chakula kama punda mwitu^e nyikani;

Huwatafutia watoto wao chakula jangwani.

6 Wanalazimika kuvuna shamba la mtu mwingine*

Na kuokota masalio katika shamba la mizabibu la mwovu.

7 Wanalala uchi usiku, bila nguo;^f

Hawana cha kujifunika ili wasipigwe na baridi.

8 Wanaloweshwa na mvua za milimani;

Wanashikilia miamba kwa

24:1 *Yaani, siku yake ya hukumu. 24:3 *Au "rehani." 24:6 *Au labda, "kuvuna chakula cha mifugo shambani."

nguvu kwa sababu hawa-
na mahali pa kujificha.

- 9** Mtoto asiye na baba
hunyakuliwa kutoka
kwenye matiti ya mama
yake;^a

Na mavazi ya maskini
huchukuliwa kuwa dha-
mana ya mkopo,^b

- 10** Na kuwalazimisha kute-
mbea uchi, bila nguo,
Wakiwa na njaa, huku
wakibeba masuke ya na-
faka.

- 11** Hufanya kazi ngumu
kwenye matuta yaliyo
milimani katika joto la
mchana; *
Hukanyaga mashinikizo ya
divai, lakini wanaona
kiu.^c

- 12** Wanaokufa wanaendelea
kulia kwa uchungu jijini;
Waliojeruhiwa vibaya sana
hulilia msaada,^d
Lakini Mungu haoni jambo
hilo kuwa baya. *

- 13** Kuna wale wanaoasi
nuru;^e
Hawatambui njia zake,
Nao hawafuati vija vyake.

- 14** Muuaji huamka wakati wa
mapambazuko;
Huwaau wasio na uwezo
na maskini,^f
Naye huiba wakati wa
usiku.

- 15** Macho ya mzinzi husubiri
giza linapoingia,^g
Akisema, 'Hakuna ataka-
yeniona!'^h

Naye huufunika uso wake.
16 Wakati wa giza wanavunja
nyumba;

24:11 * Au labda, "Hukamua mafuta kati-
kati ya kuta za matuta." **24:12** * Au lab-
da, "Mungu hamhukumu yeyote kwa ku-
tenda mabaya."

SURA YA 24

a 2Fa 4:1

b Kut 22:26, 27
Kum 24:13

c Yer 22:13
Yak 5:4

d Mhu 4:1

e Yoh 3:19

f Zb 10:4, 8

g Met 7:8-10

h 2Sa 12:9, 12
Zb 94:3, 7
Met 30:20

Safu ya 2

a Yoh 3:20

b Kum 28:15, 16
Met 3:33

c Zb 49:13, 14
Zb 55:15
Lu 12:20

d Met 10:7
Mhu 8:10
Mhu 9:5

e Mhu 8:11
Isa 56:12
Lu 12:19

f Zb 11:4
Met 5:21
Met 15:3

g Zb 37:10
Zb 92:7
Yak 1:11

h Mhu 8:12, 13

Wakati wa mchana wanaji-
fungia ndani.

Wanaepuka nuru.^a

- 17** Kwa maana kwao, asubuhi
ni kama giza zito;

Wamezoea vitisho vya giza
zito.

- 18** Lakini wanabebwa upesi
na maji. *

Fungu lao la ardhi litalaa-
niwa.^b

Hawatarudi kwenye ma-
shamba yao ya mizabibu.

- 19** Kama theluji iliyoyeyuka
inavyokaushwa na uka-
me na joto,

Ndivyo Kaburi* linavyo-
wachukua waliotenda
dhambi!^c

- 20** Mama yake atamsahau; *
naye ataliwa na mabuu.

Hatakumbukwa tena.^d

Na uovu utakatwa kama
mti.

- 21** Humwinda mwanamke
tasa,

Na kumtesa mjane.

- 22** Mungu atatumia nguvu
zake kuwaangamiza
wenye nguvu;

Hata wakiinuka, hawana
uhakika wa kuishi.

- 23** Mungu anawaacha wawe
na uhakika na wajihisi
salama,^e

Lakini macho yake yana-
tazama kila jambo
wanalotenda. *^f

- 24** Wanakwezwa kwa muda
mfupi, kisha wanato-
weka.^g

Wanashushwa chini^h na

24:18 *Tnn., "Yeye ni mwepesi juu ya
maji." **24:19** *Au "Sheoli." Angalia Ka-
musi, uku. 2012. **24:20** *Tnn., "Tu-
mbo la uzazi litamsahau." **24:23** *Tnn.,
"njia zao."

kukusanywa kama watu wengine wote;
Wanakatwa kama masuke ya nafaka.

- 25 Sasa ni nani anayeweza kuthibitisha kwamba mimi ni mwongo
Au kupinga neno langu?"

25 Bildadi^a Mshua akajibu:

- 2 "Utawala na uwezo wenye kutisha ni wake;
Yeye huimarisha amani mbinguni.*
- 3 Je, majeshi yake yanaweza kuhesabiwa?
Ni nani asiyeangaziwa na nani yake?"
- 4 Basi mwanadamu anayeweza kufa anawezaje kuwa mwadilifu mbele za Mungu,^b
Au mtu aliyezaliwa na mwanamke anawezaje kuwa bila hatia?^c
- 5 Hata mwezi si mwangavu
Na nyota si safi machoni pake,
- 6 Sembuse mwanadamu anayeweza kufa ambaye ni buu,
Na binadamu ambaye ni mnyoo!"

26 Ayubu akajibu:

- 2 "Jinsi mlivyomsaidia mtu asiye na uwezo!
Jinsi mlivyouokoa mkono usio na nguvu!^d
- 3 Kwa kweli mmempa ushauri bora mtu asiye na hekima!^e
Jinsi mlivyofunua wazi-wazi* hekima yenu inayotumika!^f

25:2 *Tnn., "katika vilele vyake." 25:4 *Au "safi." 26:3 *Au "kwa wingi."
*Au "akili yenu."

SURA YA 25

a Ayu 2:11
Ayu 8:1

b Ayu 4:17,18
Ayu 22:3

c Ayu 15:14,15

SURA YA 26

d Ayu 16:2,3

e Ayu 12:2
Ayu 17:10

Safu ya 2

a Zb 139:8
Ebr 4:13

b Ayu 9:8
Zb 104:2
Isa 42:5

c Met 30:4
Mhu 11:3

d Zb 97:2

e Met 8:27
Yer 5:22

f Zb 74:13
Isa 51:15

g Ayu 9:13

- 4 Mnajaribu kumfundisha nani,
Na ni nani aliyewaongoza msememe mambo kama hayo?*
- 5 Wale waliokufa ambao hawana uwezo hutetemeka;
Wako chini hata kuliko maji na viumbe wanao-kaa ndani yake.
- 6 Kaburi* liko uchi mbele za Mungu,^a
Na mahali pa maangamizi[#] hapajafunikwa.
- 7 Hulitandaza anga la kaskazini* mahali pasipo na kitu,^{#b}
Na kuining'iniza dunia mahali pasipo na kitu;
- 8 Huyafunga maji katika mawingu yake,^c
Ili mawingu yasisapuke kwa sababu ya uzito wake;
- 9 Hufunika kiti chake cha ufalme ili kisione kane,
Na kutandaza wingu lake juu yake.^d
- 10 Huchora upepo* juu ya maji;^e
Huweka mpaka kati ya nuru na giza.
- 11 Nguzo zenyewe za mbingu hutikisika;
Nazo hushtushwa na kemeo lake.
- 12 Huitibua bahari kwa nguvu zake,^f
Na kwa uelewaji wake huvunja vipandevipande mnyama mkubwa sana wa baharini.*^g

26:4 *Tnn., "Ni pumzi (roho) ya nani iliyotoka kwenu?" 26:6 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "Abadoni." 26:7 *Tnn., "Hutandaza kaskazini." #Au "kwenye eneo tupu." 26:10 *Tnn., "duara." 26:12 *Tnn., "Rahabu."

- 13** Kwa pumzi yake* huli-fanya anga lisiwe na mawingu;
Mkono wake humchoma nyoka anayekwepa.[#]
- 14** Tazama! Hizi ni kingo tu za njia zake;^a
Ni mnong'ono hafifu tu uliosikika kumhusu!
Basi ni nani anayeweza kuelewa mngurumo wake wenye nguvu?"^b
- 27** Ayubu akaendelea kuzungumza:*
- 2** "Kwa hakika kama Mungu anavyoishi, ambaye ameninyima haki,^c
Kama Mweza-Yote anavyoishi, ambaye amenitia uchungu,^d
- 3** Maadamu pumzi imo ndani yangu
Na roho ya Mungu imo ndani ya mianzi ya pua yangu,^e
- 4** Midomo yangu haitasema uovu;
Wala ulimi wangu hautasema udanganyifu!
- 5** Ni jambo nisiloweza kamwe kuwazia kuwatangaza ninyi kuwa waadilifu!
Mpaka nitakapokufa, sitaukana* utimilifu wangu!^f
- 6** Nitadumisha uadilifu wangu, nami sitauacha kamwe;^g
Moyo wangu hautanihukumu* maadamu ninaishi.[#]
- 7** Adui yangu na awe kama watu waovu,

26:13 *Tnn., "upepo wake." #Au "anayenyiririka." 27:1 *Tnn., "kutoa methali." 27:5 *Au "sitajiondolea; nitadumisha." 27:6 *Au "hautanidhihaki." #Au "siku yoyote maishani mwangu."

SURA YA 26

a Zb 92:5
Mhu 3:11
Isa 55:9

b Ayu 37:5

SURA YA 27

c Ayu 34:5

d Ru 1:20
2Fa 4:27

e Mwa 2:7
Isa 42:5
Mdo 17:25

f Ayu 22:1, 5
Met 27:11

g Ayu 2:3

Safu ya 2

a Ayu 13:15, 16
Ayu 36:13

b Ayu 35:12
Zb 18:37, 41
Met 28:9
Yer 11:11
Yak 4:3

c Zb 11:6
Mhu 8:13
Mal 3:5

d Est 9:7-10
Ho 9:13

Wale wanaonishambulia na wawe kama watu wasio waadilifu.

- 8** Kwa maana mtu anayemkataa Mungu* ana tumaini gani anapoangamizwa,^a
Mungu anapoondoa uhai wake?"^b
- 9** Je, Mungu atasikia kilio chake
Taabu itakapomjia?^b
- 10** Au, je, atapendezwa na Mweza-Yote?
Je, atamlilia Mungu nyakati zote?
- 11** Nitawafundisha kuhusu nguvu za* Mungu;
Sitaficha jambo lolote kumhusu Mweza-Yote.
- 12** Tazama! Ikiwa ninyi nyote mmeona maono,
Kwa nini mazungumzo yenu hayana maana yoyote?
- 13** Hilo ndilo fungu ambalo Mungu humpa mtu mwovu,^c
Urithi ambao wakandamizaji hupokea kutoka kwa Mweza-Yote.
- 14** Wanawe wakiwa wengi, watauawa kwa upanga,^d
Na wazao wake hawatakuwa na chakula cha kutosha.
- 15** Pigo litawazika wazao wake watakaobaki,
Na wajane wao hawatawaililia.
- 16** Hata akikusanya fedha kama mavumbi
Na kuhifadhi mavazi bora kama udongo wa mfi-nyanzi,

27:8 *Au "mwasi imani." #Au "nafsi yake." 27:11 *Au labda, "kwa mkono wa."

- 17** Hata akiyakusanya,
Mwadilifu ndiye atakaye-
yavaa,^a
Na wanyoofu watagawana
fedha zake.
- 18** Nyumba anayojenga ni
dhaifu kama kifuko cha
nondo,*
Kama kibanda^b kilichoje-
ngwa na mlinzi.
- 19** Ataenda kitandani akiwa
tajiri lakini hatakusanya
chochote;
Atakapofungua macho
yake, hakutakuwa na
chochote.
- 20** Hofu humkumba kama
mafuriko;
Dhoruba humnyakua
wakati wa usiku.^c
- 21** Upepo wa mashariki
utampeperusha, naye
atatoweka;
Utamfagilia mbali kutoka
mahali pake.^d
- 22** Utampiga bila huruma^e
Huku akijaribu bila mafa-
nikio kuzikimbia nguvu
zake.^f
- 23** Upepo huo humpigia ma-
kofi
Na kumpigia mluzi^g kutoka
mahali ulipo.*
- 28** "Kuna mahali pa kuchi-
mba fedha
Na mahali pa dhahabu
wanayosafisha;^h
2 Chuma hutolewa ardhini,
Na shaba huyeyushwa*
kutoka katika miamba.ⁱ
3 Mwanadamu hulishinda
giza;
Huchunguza kwa kina ka-
tika utusitusi na giza,

27:18 *Aina fulani ya wadudu waharibi-
fu. 27:23 *Au labda, "Wanampigia ma-
kofi na kumpigia mluzi kutoka mahali
pao." 28:2 *Tnn., "humwagwa."

SURA YA 27

a Met 13:22
Met 28:8
Mhu 2:26

b Isa 1:8
Omb 2:6

c Zb 73:3,19

d Mt 7:26,27

e Zb 83:15

f Isa 10:3
Amo 2:14

g Omb 2:15

SURA YA 28

h Met 17:3
Mal 3:3

i Kum 8:7,9

Safu ya 2
a 2Fa 20:20
2Nya 32:30

b Met 2:6
Yak 1:5

c Ayu 28:28

- Akitafuta mawe yenye ma-
dini.
- 4** Huzamisha bomba mbali
na makao ya watu,
Mahali paliposahauliwa,
mbali na mahali ambapo
watu wanatembea;
Wanaume fulani hushuka
wakining'inia kwa
kamba.
- 5** Chakula hukua juu
ardhini;
Lakini chini, kuna msuko-
suko kama wa moto.*
- 6** Katika mawe hayo kuna
yakuti,
Na vumbi lake lina dha-
habu.
- 7** Hakuna ndege awindaye
anayejua njia ya kufika
huko;
Jicho la mwewe mweusi
halijaiona.
- 8** Hakuna mnyama yeyote
wa mwituni mwenye
fahari aliyekanyaga;
Mwanasimba hajazunguka
huko.
- 9** Mwanadamu hugonga
mwamba mgumu kwa
mkono wake;
Huipindua milima kwenye
misingi yake.
- 10** Huchimba mitaro ya maji^a
kwenye mwamba;
Macho yake huona kila
kitu chenye thamani.
- 11** Huziba chemchemi za
mito
Na kufichua vitu vilivyofi-
chwa.
- 12** Lakini hekima—inaweza
kupatikana wapi,^b
Na kiko wapi chanzo cha
uelewaji?^c
- 13** Hakuna mwanadamu

28:5 *Inaonekana kwamba maneno
haya yanahusu uchimbaji wa madini.

- anayetambua thamani yake,^a
Nayo haiwezi kupatikana katika nchi ya walio hai.
- 14** Vilindi vya maji vinasema, 'Haimo ndani yangu!' Nayo bahari inasema, 'Haiko pamoja nami!'^b
- 15** Haiwezi kununuliwa kwa dhahabu safi; Wala thamani yake haiwezi kupimwa kwa fedha.^c
- 16** Haiwezi kununuliwa kwa dhahabu ya Ofiri^d Wala kwa madini ya shohamu na yakuti yasiyopatikana kwa urahisi.
- 17** Dhahabu na kioo haviwezi kulinganishwa nayo; Wala haiwezi kubadilishwa kwa chombo cha dhahabu bora.^{*e}
- 18** Marijani na fuwele hazi-stahili kutajwa,^f Kwa maana mfuko uliojaa hekima una thamani kuliko mfuko uliojaa lulu.
- 19** Topazi^g ya Kushi haiwezi kulinganishwa nayo; Haiwezi kununuliwa hata kwa dhahabu safi.
- 20** Lakini hekima hutoka wapi, Na kiko wapi chanzo cha uelewaji?^h
- 21** Imefichwa kutoka machoni pa kila kiumbe aliye haiⁱ Na kufichwa kutoka kwa ndege wa angani.
- 22** Maangamizi na kifo husema, 'Masikio yetu yamesikia tu habari zake.'
- 23** Mungu anaelewa njia ya kuipata;

28:17 *Au "iliyosafishwa."

SURA YA 28

a Met 3:15

b Ro 11:34

c Met 3:13, 14

d Isa 13:12

e Met 16:16

f Met 8:11
Met 20:15

g Kut 28:15, 17

h Ayu 28:12

i Mhu 8:17
1Ko 2:8, 11

Safu ya 2

a Yak 1:5

b Met 15:3
Zek 4:10
1Pe 3:12

c Zb 148:8
Mhu 1:6

d Ayu 5:10
Ayu 26:8
Ayu 37:10
Zb 135:7
Met 30:4
Isa 40:12

e Zek 10:1

f Ayu 38:25

g Kum 4:6
Zb 111:10
Met 9:10
Mhu 12:13
Ro 1:20

h Met 3:7

SURA YA 29

i Zb 18:28
Zb 119:105

j Zb 25:14
Met 3:32

Yeye peke yake ndiye anayejua inakokaa,^a

24 Kwa maana yeye hutazama mpaka kwenye miisho ya dunia, Naye huona kila kitu chini ya mbingu.^b

25 Alipoupa upepo nguvu^{*c} Na kuyapima maji,^d

26 Alipoiwekea mvua sheria^e Na njia kwa ajili ya mawingu ya dhoruba yenye ngurumo,^f

27 Kisha akaiona hekima na kuifafanua;

Aliiimarisha na kuijaribu.

28 Naye akamwambia mwanaadamu:

'Tazama! Kumwogopa Yehova—hiyo ndiyo hekima,^g

Na kuepuka uovu ni uelewaji.'^h

29 Ayubu akaendelea kuzungumza:^{*}

2 "Laiti ningekuwa kama nilivyokuwa miezi ya zamani,

Siku ambazo Mungu alikuwa akinilinda,

3 Alipoifanya taa yake inaingazie kichwani, Nilipotembea gizani kwa nuru yake,ⁱ

4 Nilipokuwa katika kilele cha mafanikio,

Urafiki pamoja na Mungu ulipohisiwa katika hema langu,^j

5 Mweza-Yote alipokuwa bado pamoja nami,

Watoto^{*} wangu wote waliponizunguka,

6 Nyayo zangu zilipoloweshwa katika siagi,

28:25 *Tnn., "uzito." 29:1 *Tnn., "ku-toa methali." 29:5 *Au "Watumishi."

- Na miamba iliponimwagia vijito vya mafuta.^a
- 7** Nilipokuwa nikienda kwenye lango la jiji^b
Na kuketi mahali pangu kwenye uwanja wa jiji,^c
- 8** Vijana walipioniona walini-pisha,*
Na hata wazee waliinuka na kuendelea kusi-mama.^d
- 9** Wakuu waliacha kuzungu-mza;
Walifunika kinywa chao kwa mkono wao.
- 10** Sauti za watu maarufu zilinyamazishwa;
Ulimi wao ulishikamana na kaaka lao.
- 11** Yeyote aliyenisikia alini-sifu,
Na wale walioniona walini-tetea.
- 12** Kwa maana nilimwoko maskini aliyelilia msaada,^e
Pamoja na yatima na yeyote ambaye hakuwa na msaidizi.^f
- 13** Mtu aliyekaribia kuangamia alinibariki,^g
Nami niliufanya moyo wa mjane ushangilie.^h
- 14** Nilivaa uadilifu kama mavazi yangu;
Haki yangu ilikuwa kama joho* na kilemba.
- 15** Nilikuwa macho kwa vipofu
Na miguu kwa walemavu.
- 16** Nilikuwa baba ya maskini;ⁱ
Nilichunguza kesi ya watu nisiowajua.^j
- 17** Nilivunja mataya ya mwovu^k

29:8 *Tnn., "waliijificha." 29:14 *Yaani, joho lisilo na mikono.

SURA YA 29

a Kum 32:13
Kum 33:24

b Ru 4:1
Met 31:23

c Ne 8:1

d Law 19:32

e Met 21:13
Met 24:11

f Yak 1:27

g Kum 24:12, 13

h Kum 10:17, 18

i Lu 14:13
Yak 1:27

j Met 29:7

k Zb 58:6
Met 30:14

Safu ya 2

a Mwa 25:8
2Fa 22:20

b Ayu 29:9

c Zb 72:6
Met 16:15

d Ayu 1:3

e Mhu 7:2

Na kuvuta mawindo kuto-ka katika meno yake.

- 18** Nilikuwa nikisema, 'Nita-fia nyumbani kwangu,*^a
Na siku zangu zitakuwa nyingi kama chembe za mchanga.
- 19** Mizizi yangu itaenea ndani ya maji,
Na umande utakaa usiku kucha kwenye matawi yangu.
- 20** Utukufu wangu hufanywa kuwa mpya daima,
Na upinde ulio mkononi mwangu utaendelea kupiga mishale.'
- 21** Watu walisikiliza kwa hamu,
Walingojea kimyakimya ushauri wangu.^b
- 22** Nilipomaliza kuongea, hawakuwa na la kuongeza;
Maneno yangu yalipenya taratibu* masikioni mwao.
- 23** Waliningojea kama wana-vyongojea mvua;
Walifumbua vinywa vyao wazi kana kwamba wanangojea mvua ya masika.^c
- 24** Nilipotabasamu, hawa-kuamini;
Nuru ya uso wangu iliwapa ujasiri.*
- 25** Niliwapa mwelekezo niki-wa kiongozi wao,
Nami niliishi kama mfalme anayezungukwa na majeshi yake,^d
Kama mtu anayewafariji waombolezaji.^e

29:18 *Tnn., "kwenye kiota changu."

29:22 *Tnn., "yalitonatona."

29:24 *Au labda, "Hawakuitia giza nuru ya uso wangu."

- 30** “Sasa wananicheka^a
—Wanaume wenye umri
mdogo kuliko mimi,
Ambao baba zao ninge-
kataa
Kuwaweka pamoja na
mbwa waliolinda kondoo
wangu.
- 2** Nguvu za mikono yao
zilikuwa na faida gani
kwangu?
Nguvu zao zimekwisha.
- 3** Wamedhoofika kwa saba-
bu ya umaskini na njaa;
Wanaguguna ardhi iliyo-
kauka
Ambayo ilikuwa tayari
imeharibiwa na kuachwa
ukiwa.
- 4** Wanakusanya mmea we-
nye chumvi kutoka
vichakani;
Chakula chao ni mizizi ya
miretemu.
- 5** Wanafukuzwa kutoka kati-
ka jamii;^b
Watu wanawapigia kelele
kama wanavyompigia ke-
lele mwizi.
- 6** Wanaishi kwenye mitere-
mko ya mabonde,*
Kwenye mashimo ardhini
na katika miamba.
- 7** Wanalia kwa sauti kutoka
vichakani
Na kujikunyata pamoja ka-
tikati ya upupu.
- 8** Kama wana wa watu wa-
pumbavu na wasio na
jina,
Wamefukuzwa* kutoka
nchini.
- 9** Lakini sasa wananidhiha-
ki hata katika nyimbo
zao;^c

30:6 *Au “makorongo.” 30:8 *Tnn.,
“Wamepigwa mijeledi na kufukuzwa.”

SURA YA 30

a Ayu 12:4

b Mwa 4:12
Zb 109:10
Da 4:25c Zb 69:12
Omb 3:14

Safu ya 2

a Ayu 17:6

b Ayu 19:13

c Hes 12:14
Kum 25:9
Isa 50:6
Mt 27:30d Ayu 16:2
Zb 69:26

e Zb 22:14

f Ayu 10:15

g Zb 6:2

h Ayu 2:8,13
Ayu 7:4

Nimekuwa kitu cha kudha-
rauliwa nao.*^a

- 10** Wananichukia na kukaa
mbali nami;^b
Hawasiti kunitemea mate
usoni.^c
- 11** Kwa sababu Mungu ame-
nidhoofisha* na
kuninyenyekeza,
Wanafanya watakavyo[#]
mbele zangu.
- 12** Wanainuka upande wangu
wa kulia kama umati;
Wananimbiza
Na kuweka vizuizi vya
maangamizi kwenye njia
yangu.
- 13** Wanaharibu barabara
zangu
Na kuzidisha msiba wa-
ngu,^d
Na hakuna yeyote anaye-
wazuia.*
- 14** Wanakuja kana kwamba
wanapita kwenye ufa
mpana ukutani;
Wanamiminika ndani
katikati ya magofu.
- 15** Hofu inanilemea;
Heshima yangu inapeperu-
shwa mbali kama upepo,
Na wokovu wangu unato-
weka kama wingu.
- 16** Sasa uhai wangu unatowe-
ka taratibu;^e
Siku za mateso^f zinashika-
mana nami.
- 17** Maumivu yanatoboa mifu-
pa yangu* usiku;^g
Na maumivu yanayonita-
funa hayaishi kamwe.^h

30:9 *Tnn., “methali; msemu kwao.”

30:11 *Tnn., “amelegeza kamba ya
upinde wangu.” [#]Tnn., “Wanatulipia
mbali lijamu.” 30:13 *Au labda, “Na
hakuna yeyote anayewasaidia.” 30:17
*Tnn., “Mifupa yangu inatobolewa.”

- 18** Kwa nguvu nyingi vazi langu limechakazwa;* Hunikaba kama ukosi wa vazi langu.
- 19** Mungu ameniangusha chini kwenye matope; Nimebaki mavumbi na majivu tu.
- 20** Ninakulilia unisaidie, lakini hunijibu;^a Ninasimama, lakini unaniangalia tu.
- 21** Umenigeukia kwa ukatili;^b Kwa nguvu zote za mkono wako, unanishambulia.
- 22** Unaiinua juu na kunipeperusha katika upepo; Kisha unanitupa huku na huku katika dhoruba.*
- 23** Kwa maana ninajua kwamba utanishusha katika kifo, Katika nyumba ambamo watu wote walio hai watakutana.
- 24** Lakini hakuna yeyote anayeweza kumshambulia mtu anayetaabika*^c Anapolilia msaada wakati wa msiba.
- 25** Je, sijawalilia wale ambao wamekabili nyakati ngumu?* Je, sijawahuzunikia maskini?^d
- 26** Ingawa nilitumaini mema, mabaya yalikuja; Nilitarajia nuru, lakini giza likaja.
- 27** Msukusuko uliokuwa ndani yangu haukukoma; Siku za mateso zilinikabili.

30:18 *Au labda, "Mateso yangu makali yanauharibu mwili wangu." **30:22** *Au labda, "unaniyeyusha kwa kishindo." **30:24** *Tnn., "kushambulia rundo la magofu." **30:25** *Au "walio na siku ngumu?"

SURA YA 30

a Ayu 19:7
Zb 22:2

b Ayu 7:20
Ayu 19:6

c Ayu 13:25

d Met 14:21
Met 14:31
Met 19:17

Safu ya 2

a Zb 38:6
Zb 42:9
Zb 43:2

b Mik 1:8

c Ayu 7:5
Omb 4:8

SURA YA 31

d Met 6:25, 26
Mt 5:28

e Ayu 31:9, 10

f Ayu 20:26-29
Zb 73:3, 18
Met 10:29

g Mwa 16:13
2Nya 16:9
Zb 139:3
Met 5:21
Yer 32:19

h Zb 26:5
Met 6:16, 18

i 1Sa 2:3

- 28** Ninatembeatembea kwa huzuni;^a hakuna mwangaza wa jua. Ninasimama na kulilia msaada katika kusanyiko.
- 29** Nimekuwa ndugu ya mbwamwitu Na rafiki ya mabinti wa mbuni.^b
- 30** Ngozi yangu imekuwa nyeusi na imebambuka;^c Mifupa yangu inaungua kwa sababu ya joto.*
- 31** Kinubi changu kinatumika kwa ajili ya maombolezo tu, Na zumari* yangu kwa ajili ya sauti ya kilio.
- 31** "Nimefanya agano na macho yangu.^d Basi ninawezaje kumtazama bikira kwa njia isiyofaa?^e
- 2** Basi, nitapata fungu gani kutoka kwa Mungu aliye juu, Urithi gani kutoka kwa Mweza-Yote aliye juu?
- 3** Je, msiba haumngojei mkosaji Na maafa wale wanaofanya mambo yanayodhuru?^f
- 4** Je, yeye haoni njia zangu^g Na kuhesabu hatua zangu zote?
- 5** Je, nimewahi kutembea katika njia isiyo ya kweli?*" Je, mguu wangu umekimbilia udanganyifu?^h
- 6** Mungu na anipime kwa mizani sahihi;ⁱ

30:30 *Au labda, "homa." **30:31** *Au "filimbi." **31:5** *Au labda, "na watu wasiopenda kweli?"

Ndipo atakapotambua utimilifu wangu.^a

- 7 Hatua zangu zikikengeuka kutoka kwenye njia^b

Au ikiwa moyo wangu umefuata macho yangu^c
Au ikiwa mikono yangu imechafuliwa,

- 8 Basi acha nipande mbegu na mtu mwingine ale,^d
Na acha mimea ninayopanda ing'olewe.*

- 9 Ikiwa moyo wangu umeshawishiwa na mwanamke^e

Nami nimenyemelea^f kati-ka mlango wa jirani yangu,

- 10 Basi acha mke wangu amsagie nafaka mwanaume mwingine,
Na acha wanaume wengine wafanye ngono naye.*^g

- 11 Kwa maana hilo lingekuwa tendo la aibu,
Kosa linalostahili adhabu kutoka kwa waamuzi.^h

- 12 Ungekuwa moto unaoteke-teza na kuangamiza,*ⁱ
Unaoteketeza hata mizizi ya[#] mazao yangu yote.

- 13 Ikiwa niliwanyima haki watumishi wangu wa kiu-me na wa kike
Walipokuwa na malalami-ko* dhidi yangu,

- 14 Nitafanya nini Mungu aki-nikabili?*
- Nitamjibu nini akinifanya niwajibike?^j

- 15 Je, Yule aliyeniumba tumboni mwa mama

31:8 *Au "acha wazao wangu wang'olewe." 31:10 *Tnn., "acha wanaume wengine wapige magoti juu yake." 31:12 *Tnn., "unaokula (unaonyafua) na kuangamiza." #Au "Unaong'oa." 31:13 *Au "kesi." 31:14 *Tnn., "akiinuka?"

SURA YA 31

a Ayu 2:3
Ayu 27:5
Zb 7:8

b Kum 11:16
Yer 10:23

c Hes 15:39
Mhu 11:9
Eze 6:9
Mt 5:29
IYo 2:16

d Law 26:16

e Ayu 31:1
Mt 5:28

f Ayu 24:15

g 2Sa 12:9,11
Yer 8:10

h Mwa 38:24
Law 20:10
Kum 22:22

i Met 6:25-27
Met 7:27

j Met 22:22, 23
Isa 10:1-3

Safu ya 2

a Ayu 34:19
Met 14:31
Met 22:2
Mal 2:10

b Zb 139:16

c Kum 15:7, 8

d Kum 10:18
Met 28:27

e Eze 18:5, 7
Yak 1:27
IYo 3:17

f Isa 58:7
Lu 3:11
Yak 2:15, 16

g Kum 24:13

h Met 14:21

i Met 31:23

yangu hakuwaumba wao pia?^a

Je, si Ndiye aliyetuumba sisi kabla hatujazaliwa?^{*b}

- 16 Ikiwa nilikataa kuwapa maskini walichotamani^c

Au ikiwa niliyahuzunisha macho ya mjane,*^d

- 17 Ikiwa nilikula chakula changu peke yangu
Bila kuwagawia mayatima;^e

- 18 (Kwa maana tangu nilipokuwa kijana, nimemlea yatima kana kwamba mimi ni baba yake,
Nami nimekuwa kiongozi wa mjane tangu utotoni.*)

- 19 Ikiwa nilimwona yeyote akiangamia kwa kukosa mavazi

Au maskini asiye na chochote cha kujifunika;^f

- 20 Ikiwa hakunibariki*^g
Alipokuwa akijipasha joto kwa manyoya ya kondoo wangu;

- 21 Ikiwa nilitikisa ngumi yangu na kumtisha yatima^h
Alipohitaji msaada wangu kwenye lango la jiji;*ⁱ

- 22 Basi acha mkono* wangu ung'oke kutoka begani mwangu,
Na acha mkono wangu uvunjwe kwenye kiwiko[#] chake.

31:15 *Tnn., "katika tumbo la uzazi."

31:16 *Tnn., "niliyadhoofisha macho ya mjane." 31:18 *Tnn., "tangu tumboni mwa mama yangu." 31:20 *Tnn., "ikiwa kiuno chake hakikunibariki." 31:21 *Au labda, "Nilipoona kwamba nina watu wanaonisaidia katika lango la jiji." 31:22 *Au "mtulinga." #Au "kwenye kiungio chake; kutoka kwenye mfupa wake wa juu."

- 23** Kwa maana niliogopa sana msiba kutoka kwa Mungu, Nami sikuweza kustahimili adhama yake.
- 24** Ikiwa nilifanya dhahabu kuwa tumaini langu Au kuiambia dhahabu bora, 'Wewe ni mlinzi wangu!'^a
- 25** Ikiwa shangwe yangu ilikuwa utajiri wangu mwingi^b Kwa sababu ya mali nyingi nilizokusanya;^c
- 26** Ikiwa niliona jua liking'aa* Au mwezi ukizunguka kwa fahari yake;^d
- 27** Na moyo wangu ukashawishiwa kwa siri, Na kinywa changu kika-busu mkono wangu nikiviabudu;^e
- 28** Basi hilo ni kosa linalostahili adhabu kutoka kwa waamuzi, Kwa maana nitakuwa ni-memkana Mungu wa kweli aliye juu.
- 29** Je, nimewahi kushangilia kuangamizwa kwa adui yangu^f Au kumcheka kwa sababu amepatwa na uovu?
- 30** Sikuruhusu kamwe kinywa changu kitende dhambi Kwa kuapa kwamba afe.^g
- 31** Je, watu wa hema langu hawajauliza, 'Ni nani anayeweza kum-pata mtu ambaye hajashibishwa na chakula chake?'^{*h}

31:26 *Tnn., "nuru iking'aa." **31:31** *Tnn., "nyama yake."

SURA YA 31

a Zb 49:6,7
1Ti 6:17

b Est 5:11
Zb 62:10
Met 11:28

c Kum 8:17,18

d Kum 4:19

e Kum 11:16

f Met 17:5
Met 24:17,18

g Mt 5:44
Ro 12:14

h Mwa 18:5
Ro 12:13

Safu ya 2

a Mwa 19:1,3
Ebr 13:2
1Pe 4:9

b Mwa 3:8
Met 28:13
Mdo 5:8

c Ayu 19:7

d Ayu 13:22

e Yak 5:4

f 1Fa 21:15

- 32** Hakuna mgeni* aliyelazimika kulala nje usiku;^a Nilimfungulia milango msafiri.
- 33** Je, nimewahi kujaribu kufunika dhambi zangu, kama watu wengine,^b Kwa kuficha uovu wangu katika mfuko wa vazi langu?
- 34** Je, nimewahi kuogopa umati utakavyotenda, Au kutishwa na dharau za familia nyingine, Na hivyo kukaa kimya na kuogopa kutoka nje?
- 35** Laiti mtu fulani angenisi-kiliza!^c Ningeweka sahihi ya jina langu kwenye mambo niliyosema!^{*} Mweza-Yote na anijibu!^d Laiti mshtaki wangu angeandika mashtaka yangu kwenye hati!
- 36** Ningeibebea begani mwangu, Nami ningeifunga kama taji kuzunguka kichwa changu.
- 37** Ningempa habari kuhusu kila hatua niliyopiga; Ningemfikia kwa ujasiri, kama kiongozi.
- 38** Ikiwa ardhi yangu mwe-nyewe ingetoa kilio dhidi yangu Na mitaro yake ingelia pa-moja;
- 39** Ikiwa nimekula mazao yake bila kulipa,^e Au ikiwa nimewakatisha tamaa wamiliki wake;^f
- 40** Basi miiba ichipuke kwa ajili yangu badala ya ngano

31:32 *Au "mkaaji mgeni." **31:35** *Au "Hii ndiyo sahihi yangu."

Na magugu yenye harufu mbaya badala ya shayiri.”

Maneno ya Ayubu yanai-shia hapa.

32 Basi wanaume hao watatu wakaacha kumjibu Ayubu, kwa sababu alisadiki kwamba yeye ni mwadilifu.*^a **2** Lakini Elihu mwana wa Barakeli, kutoka Buzi,^b wa ukoo wa Ramu, akakasirika sana. Hasira yake iliwa-ka dhidi ya Ayubu kwa sababu alijaribu kujithibitisha mwenyewe kuwa mwadilifu bada-la ya Mungu.^c **3** Pia, aliwakasirikia vikali marafiki watatu wa Ayubu kwa sababu walishindwa kujibu lakini walikuwa wamemtangaza Mungu kuwa mwovu.^d **4** Elihu alikuwa amesubiri kumjibu Ayubu, kwa sababu walikuwa na umri mkubwa kuliko yeye.^e **5** Elihu alipoona kwamba wanaume hao watatu hawakuwa na jambo la kusema, aliwaka hasira. **6** Kwa hiyo Elihu mwana wa Barakeli, kutoka Buzi, akaanza kuzungumza, akasema:

“Mimi ni kijana*^f

Lakini ninyi ni wazee.^f

Kwa hiyo kwa heshima nilijizuia,^g

Nami sikuthubutu kuwaambia ninayojua.

7 Niliwaza, ‘Acha umri uzungumze,*

Na acha wingi wa miaka utangaze hekima.’

8 Lakini ni roho iliyo ndani ya watu,

Pumzi ya Mweza-Yote, inayowapa uelewaji.^h

SURA YA 32

a Ayu 6:29
Ayu 27:6

b Mwa 22:20, 21

c Ayu 10:2, 3

d Kut 20:7
Ayu 4:18-20
Ayu 22:2, 3
Ayu 25:5, 6
Ayu 42:8

e Law 19:32

f Ayu 15:10

g ITi 5:1
Ipe 5:5

h IFa 3:12
IFa 4:29
Ayu 35:11
Met 2:6
Mhu 2:26
Da 1:17
Mt 11:25
Yak 1:5

Safu ya 2

a Zb 119:100
Mhu 4:13

b Yak 1:19

c Met 15:28

9 Umri peke yake haumfany* mtu awe na hekima, Wala si wazee peke yao wanaolewa yaliyo sawa.^a

10 Kwa hiyo ninasema, ‘Nisikilizeni, Nami pia nitawaambia ninayojua.’

11 Tazameni! Nimesubiri maneno yenu; Niliendelea kusikiliza hoja zenu^b

Mlipokuwa mkitafuta mambo ya kusema.^c

12 Niliwasikiliza kwa makini, Lakini hakuna yeyote miongoni mwenu aliyeweza kuthibitisha kwamba Ayubu amekosea*^d

Wala kujibu hoja zake.

13 Kwa hiyo msiseme, ‘Tumepata hekima; Mungu ndiye anayempinga, si mwanadamu.’

14 Ayubu hakuelekeza maneno yake kwangu, Kwa hiyo sitamjibu kwa kutumia hoja zenu.

15 Wamefadhika, hawana mambo zaidi ya kusema; Wameishiwa na maneno.

16 Nimesubiri, lakini hawaindelei kuzungumza; Wamesimama pale tu, hawana majibu zaidi.

17 Basi, mimi pia nitajibu; Mimi pia nitasema ninayojua,

18 Kwa maana nina mengi ya kusema; Roho iliyo ndani yangu inanishurutisha.

19 Matumbo yangu ni kama divai isiyo na mahali pa kutokea,

32:1 *Au “alijiona kuwa mwadilifu.”
32:6 *Tnn., “Mimi ni mdogo wa siku.”
32:7 *Tnn., “siku ziseme.”

32:9 *Au “Siku nyingi peke yake hazimfanyi.” 32:12 *Au “aliyeweza kumkaripia Ayubu.”

Kama viriba vipya vya divai vinavyokaribia kupasuka.^a

20 Acha nizungumze ili nipate kitulizo!

Nitafungua midomo yangu na kujibu.

21 Sitampendelea yeyote;^b Wala kumsifusifu* mwana-damu yeyote,

22 Kwa maana sijui kusifu-sifu;

Nikifanya hivyo, Muumba wangu ataniangamiza.

33 “Lakini sasa, Ayubu, tafadhali sikiliza maneno yangu;

Sikiliza kila jambo nitakalosema.

2 Tazama, tafadhali! Ni lazima nifumbue kinywa changu;

Ni lazima ulimi wangu uzungumze.*

3 Maneno yangu yanatanga za unyoofu wa moyo wangu,^c

Na midomo yangu inasema kwa unyoofu mambo ninayojua.

4 Roho ya Mungu mwenyewe iliniumba,^d

Na pumzi ya Mweza-Yote mwenyewe ilinifanya niwe hai.^e

5 Nijibu ikiwa unaweza; Niambie hoja zako; jitayarisha kujitetea.

6 Tazama! Mimi ni kama wewe mbele za Mungu wa kweli;

Mimi pia niliumbwa kwa udongo.^f

7 Kwa hiyo usiniogope,

SURA YA 32

a Mt 9:17

b Law 19:15
Met 24:23
Yak 3:17

SURA YA 33

c Mt 12:34
Lu 6:45

d Zb 119:73

e Mwa 2:7
Mhu 12:7
Mdo 17:25

f Mwa 2:7

Safu ya 2

a Ayu 10:7
Ayu 16:16,17
Ayu 23:11

b Ayu 29:14

c Ayu 12:34
Ayu 16:9
Ayu 19:11

d Ayu 13:27
Ayu 14:16
Ayu 31:4

e Ayu 12:13
Zb 8:4
Isa 40:25
Isa 55:9

f Isa 45:9
Ro 9:20

g Ayu 13:24

h Hes 12:6
Da 4:5

i Ayu 36:10

j Mwa 20:6,7
Mt 27:19

k Da 4:24,25

l Mwa 31:24

Na uzito wa maneno yangu usikulemee.

8 Lakini nilisikia ukisema, Naam, niliendelea kusikia maneno haya,

9 ‘Mimi ni safi, sina dhambi;^a

Mimi ni safi, sina kosa.^b

10 Lakini Mungu anatafuta sababu za kunipinga; Ananiona kuwa adui yake.^c

11 Anaitia miguu yangu kati-ka mikatale; Anavichunguza kwa maki-ni vijia vyangu vyote.^d

12 Lakini umekosea kusema hivyo, kwa hiyo nitakujibu:

Mungu ni mkuu sana kuliko mwanadamu anayeweza kufa.^e

13 Kwa nini unamlaumu Yeye?^f

Je, ni kwa sababu hakuji-bu hoja zako zote?^g

14 Kwa maana Mungu huzunguma mara moja na mara ya pili,

Lakini hakuna yeyote ana-yesikiliza,

15 Huzungumza katika ndoto, maono ya usiku,^h Watu wanaposhikwa na usingizi mzito

Wanapolala vitandani mwao.

16 Kisha hufungua masi-kio yaoⁱ Na kuyakazia* maagizo yake kwao,

17 Ili kumwepusha mtu asite-nde dhambi/

Na kumlinda mwanadamu asiwe na kiburi.^k

18 Mungu huilinda nafsi yake isiingie* shimoni,^l

32:21 *Au “kumpa ulima la cheo.” 33:2 *Tnn., “Ni lazima ulimi wangu na kaaka langu vizungumze.”

33:16 *Tnn., “kuyatia muhuri.” 33:18 *Au “huilinda uhai wake usiingie.” #Au “kaburini.”

- Uhai wake usiangamizwe kwa upanga.*
- 19** Mtu hukaripiwa pia na maumivu kitandani mwake
Na mateso yasiyo na kiko-mo mifupani mwake,
- 20** Hivi kwamba nafsi yake inachukia* mkate, Naye anakataa hata chakula bora.^a
- 21** Nyama ya mwili wake huisha hivi kwamba haionekani,
Na mifupa yake iliyokuwa imefichika sasa imecho-moza.*
- 22** Nafsi yake inakaribia* shimoni;#
Uhai wake unawakaribia wale wanaoleta kifo.
- 23** Ikiwa kuna mjumbe* kwa ajili yake,
Mtetezi mmoja kati ya elfu moja,
Ili amwambie mwanadamu mambo manyoofu,
- 24** Basi Mungu humhurumia na kusema,
'Mwokoe asishuke shi-
moni!#^b
Nimepata fidia!'^c
- 25** Mwili wake na uwe na afya zaidi kuliko wakati wa ujana;^d
Na azirudie siku alizokuwa na nguvu za ujana.'^e
- 26** Atamsihi Mungu,^f naye atamkubali,
Naye ataona uso wa Mungu kwa kelele za shangwe,

33:18 *Au "kwa silaha." **33:20** *Tnn., "uhai wake unachukia." **33:21** *Au "inaonekana waziwazi." **33:22** *Au "Uhai wake unakaribia." **33:22, 24, 28, 30** #Au "kaburini." **33:23** *Au "ma-laika."

SURA YA 33

a Zb 107:17, 18

b Ayu 14:13

c Ayu 19:25
Mt 20:28

d 2Fa 5:14

e Kum 34:7
Ayu 42:16
Zb 103:3-5

f Zb 30:8

Safu ya 2

a 2Sa 12:13
Zb 32:5
Met 28:13
Lu 15:21
1Yo 1:9b Zb 19:14
Isa 38:17

c Zb 56:13

- Na Mungu atamrudishia uadilifu Wake mwanadamu anayeweza kufa.
- 27** Mtu huyo atawatangazia* wanadamu,
'Nimetenda dhambi^a na kupotosha yaliyo sawa, Lakini sikupokea niliyo-stahili.#
- 28** Ameikomboa nafsi yangu isiingie* shimoni,^{#b}
Na uhai wangu utaona nuru.'
- 29** Kwa kweli, Mungu hufanya mambo haya yote Mara mbili, mara tatu, kwa ajili ya mwanadamu,
- 30** Ili kumrudisha kutoka shi-
moni,#
Ili aweze kuangaziwa nuru ya uzima.^c
- 31** Sikiliza, Ayubu! Nisikilize! Nyamaza, nami nitaendelea kuzungumza.
- 32** Ikiwa una jambo la kusema, niambia.
Sema, kwa maana nataka kuthibitisha kwamba uko sahihi.
- 33** Ikiwa huna la kusema, unapaswa kunisikiliza; Nyamaza, nami nitakufundisha hekima."
- 34** Kwa hiyo, Elihu akaendelea kusema:
- 2** "Sikilizeni maneno yangu, ninyi mlio na hekima; Nisikilizeni, ninyi mnaojua mambo mengi sana.
- 3** Kwa maana sikio hupima maneno
Kama ulimi unavyoonja* chakula.

33:27 *Tnn., "atawaimbia." #Au labda, "Nami sikupata faida." **33:28** *Au "Ameukomboa uhai wangu usiingie." **34:3** *Tnn., "kaakaa linavyoonya."

- 4 Acheni tuchanganue wenyewe yaliyo sawa; Acheni tuamue miongoni mwetu yaliyo mema.
- 5 Kwa maana Ayubu amesema, 'Sijakosea,^a Lakini Mungu ameninyima haki.^b
- 6 Je, ninaweza kusema uwongo kuhusu hukumu ninayostahili? Kidonda changu hakiponi, ingawa sina kosa.^c
- 7 Ni nani aliyekama Ayubu, Anayekunywa dharau kama maji?
- 8 Yeye ni rafiki ya watenda dhambi Naye hushirikiana na waovu.^d
- 9 Kwa maana amesema, 'Mwanadamu hafaidiki Kwa kujitahidi kumpendelea Mungu.^e
- 10 Kwa hiyo nisikilizeni, ninyi watu wenye uelewaji.* Mungu wa kweli hawezi kamwe kuwazia kutenda uovu,^f Na Mweza-Yote hawezi kamwe kutenda kosa!^g
- 11 Kwa maana atamlipa mwanadamu kulingana na matendo yake^h Na kumletea matokeo ya njia zake.
- 12 Kwa hakika, Mungu hate-ndi uovu;ⁱ Mweza-Yote hapotoshi haki.^j
- 13 Ni nani aliyempa mamlaka ya kusimamia dunia, Na ni nani aliyemweka asimamie ulimwengu mzima?*

34:10 *Tnn., "moyo." 34:13 *Au "dunia inayokaliwa."

SURA YA 34

- a Ayu 29:14
Ayu 33:9
- b Ayu 27:2
- c Ayu 9:17, 18
- d Met 1:10, 15
Met 4:14
- e Ayu 9:22-24
Ayu 35:3
- f Mwa 18:25
2Nya 19:7
Zb 92:15
- g Kum 32:4
Ro 9:14
Ebr 6:10
- h 1Nya 28:9
Zb 62:12
Met 24:12
Yer 32:19
Eze 33:20
Ro 2:6
ZKo 5:10
Gal 6:7
1Pe 1:17
Ufu 22:12
- i Yak 1:13
- j Zb 89:14
Zb 97:2
Zb 99:4
Ro 2:11

Safu ya 2

- a Zb 104:29
Mhu 12:7
Isa 42:5
Mdo 17:25
- b Mwa 3:19
Zb 146:4
Mhu 3:20
- c Kut 22:28
Mhu 8:2-4
Mhu 10:20
- d Kum 10:17
2Nya 19:7
Mdo 10:34
Ro 2:11
Efe 6:9
- e Ayu 31:13-15
Met 22:2
- f Zb 73:3, 19
Mdo 12:21-23
- g Kut 12:29
Da 5:30
- h 1Sa 25:38
- i Mwa 6:5
2Nya 16:9
Ayu 31:4
Met 5:21
Met 15:3
Yer 16:17
Yer 32:19
1Pe 3:12
- j Zb 139:11, 12
Isa 29:15
Yer 23:24
Amo 9:3
Ebr 4:13

- 14 Akiwakazia fikira,* Akijikusanyia roho yao na pumzi yao,^a
- 15 Wanadamu wote wataa-
ngamia* pamoja,
Nao watarudi mavumbini.^b
- 16 Basi ikiwa mna uelewaji,
sikilizeni mambo haya;
Sikilizeni kwa makini
ninayosema.
- 17 Je, mtu anayechukia haki
anapaswa kuongoza,
Au je, mtamhukumu mwe-
nye nguvu ambaye ni
mwadilifu?
- 18 Je, mtamwambia mfalme,
'Wewe hufai kitu,'
Au viongozi, 'Ninyi ni
waovu'?^c
- 19 Kuna Yule asiyewapende-
lea wakuu
Na ambaye hawapendelei
matajiri na kuwapuuzia
maskini,^{*d}
Kwa maana wote ni kazi ya
mikono yake.^e
- 20 Wanaweza kufa ghafla,^f
katikati ya usiku;^g
Wanatikisika kwa nguvu
na kufa;
Hata wenye nguvu
huondolewa, lakini
si kwa mikono ya
wanadamu.^h
- 21 Kwa maana yao
Mungu hutazama njia
za mwanadamu,ⁱ
Naye huziona hatua zake
zote.
- 22 Hakuna giza wala kivuli
kizito
Ambamo watenda maovu
wanaweza kujificha.^j

34:14 *Tnn., "moyo wake." 34:15
*Tnn., "Mili yote itaangamia." 34:19
*Au "watu maarufu na kuwapuuzia watu
wa hali ya chini."

- 23** Kwa maana Mungu haja-weka wakati hususa wa mwanadamu yeyote Kufika mbele zake ili ahukumiwe.
- 24** Huwapondaponda wenye nguvu bila kuhitaji kufanya uchunguzi Na kuwaweka wengine mahali pao.^a
- 25** Kwa maana anajua wana-yofanya,^b Huwapindua wakati wa usiku, nao huangami-zwa.^c
- 26** Huwapiga kwa sababu ya uovu wao, Mahali ambapo watu wote wanaweza kuona,^d
- 27** Kwa sababu wameacha kumfuata^e Nao hawaheshimu yoyote kati ya njia zake;^f
- 28** Wanasababisha maskini wamililie, Hivi kwamba anasikia kilio cha wasio na uwezo.^g
- 29** Mungu akikaa kimya, ni nani anayeweza kumshutumu? Akiuficha uso wake, ni nani anayeweza kumwona? Iwe ni kwa taifa au mtu mmoja, matokeo ni yale-yale,
- 30** Ili mtu anayemkataa Mungu* asitawale^h Au kuwawekea wengine mitego.
- 31** Je, kuna yeyote anayeweza kumwambia Mungu, 'Nimeadhibiwa, ingawa sijafanya kosa lolote;ⁱ
- 32** Nifundishe jambo ambalo nimeshindwa kuona;

34:30 *Au "mwasi imani."

SURA YA 34

a Eze 21:26, 27
Da 2:21
Da 4:25

b Ho 7:2

c 1Sa 4:17
Da 5:30

d Hes 12:10

e 1Sa 15:11

f Zb 28:5

g Kut 22:22, 23
Yak 5:4

h Ayu 13:16
Ayu 27:8

i Da 9:7
Ro 3:23

Safu ya 2

a Ayu 35:16
Ayu 38:2
Ayu 42:3

b Ayu 10:1
Ayu 19:6

c Ayu 35:2

SURA YA 35

d Ayu 10:7
Ayu 16:16, 17
Ayu 34:5

e Ayu 9:22-24
Ayu 34:9
Zb 73:13

f Ayu 2:11

g Zb 68:34

Ikiwa nimetenda kosa lolote, sitalirudia tena?'

- 33** Je, akuthawabishe kwa masharti yako wakati unakataa hukumu yake? Amua mwenyewe, si mimi. Basi niambie mambo unayojua vema.
- 34** Watu wenye ulewaji* wataniambia —Mtu yeyote mwenye hekima anayenisikiliza—
- 35** 'Ayubu anazungumza bila ujuzi,^a Na maneno yake hayana ufahamu.'
- 36** Acha Ayubu ajaribiwe* kikamili Kwa sababu majibu yake ni kama ya watu waovu!
- 37** Anaongeza uasi kwenye dhambi yake;^b Anapiga makofi kwa dharau mbele yetu Na kusema maneno mengi dhidi ya Mungu wa kweli!"^c
- 35** Elihu akaendelea kusema:
- 2** "Je, unasadiki kabisa kwamba uko sahihi hivi kwamba unasema, 'Mimi ni mwadilifu kuliko Mungu?'"^d
- 3** Kwa maana unasema, 'Hilo linakuhusuje?*' Je, hali yangu ni bora kuliko kama ningetenda dhambi?'"^e
- 4** Nitakujibu wewe Na rafiki zako^f walio pamoja nawe.
- 5** Tazama mbinguni uone, Yaangalie mawingu,^g

34:34 *Tnn., "moyo." **34:36** *Au labda, "Baba yangu, acha Ayubu ajaribiwe." **35:3** *Inaelekea anamwambia Mungu.

ambayo yako mbali sana juu yako.

- 6** Ukitenda dhambi, unamuumizaje?^a
Dhambi zako zikiongeze-ka, unamwathirije?^b
- 7** Ukiwa mwadilifu, unampa nini;
Anapokea nini kutoka kwako?^c
- 8** Uovu wako unamwathiri tu mwanadamu kama wewe,
Na uadilifu wako, bina-damu.
- 9** Watu hulia kwa sauti wanapokandamizwa sana;
Wanalia wapate kitulizo kutoka chini ya mamlaka ya * wenye nguvu.^d
- 10** Lakini hakuna anayeuliza, 'Yuko wapi Mungu, Muumba wangu Mkuu,^e
Yule anayesababisha nyimbo ziimbwe usiku?'^f
- 11** Hutufundisha^g kuliko wanyama mwitu wa dunia,^h
Naye hutufanya tuwe na hekima kuliko ndege wa angani.
- 12** Watu hulia kwa sauti, laki-ni Yeye hajibu,ⁱ
Kwa sababu ya kiburi cha waovu.^j
- 13** Kwa kweli Mungu hasikilizi kilio kisicho na maana,^{*k}
Mweza-Yote hakisikilizi.
- 14** Sembuse wewe unapolalameka kwamba humwoni!
Kesi yako iko mbele zake, kwa hiyo unapaswa kumngojea kwa hamu.^m
- 15** Kwa maana hajakuadhibu kwa hasira;

35:9 *Tnn., "kutoka mkononi mwa."
35:13 *Au "hasikilizi uwongo."

SURA YA 35

- a Met 8:36
Met 9:12
- b Met 19:3
- c Ro 11:35
- d Met 29:2
- e Isa 51:12, 13
1Pe 4:19
- f Zb 42:8
Zb 149:5
Mdo 16:25
- g Zb 94:12
Isa 48:17
- h Mwa 1:26
- i Zb 18:41
- j Met 1:28, 29
1Pe 5:5
- k Met 15:29
Isa 1:15
Yer 11:11
- l Ayu 9:11
- m Zb 37:5

Safu ya 2

- a Zb 103:10-12
- b Ayu 34:35
Ayu 38:2

SURA YA 36

- c Kum 32:4
Zb 11:7
Zb 139:14
Da 9:14
Ufu 15:3
- d 1Sa 2:3
Ayu 37:16
- e Zb 24:8
Zb 99:4
Yer 32:18
- f Zb 9:17
Zb 68:2
2Pe 2:9
- g Zb 10:14
Zb 140:12
Met 22:22, 23
- h Zb 33:18
Zb 34:15
- i Zb 78:70, 71
Zb 113:7, 8
Isa 9:7

Wala hajakazia fikira maneno unayosema haraka-haraka bila kufikiri.^a

- 16** Ayubu hufumbua kinywa chake wazi kwa ubatili; Huongea maneno mengi bila ujuzi."^b

36 Elihu akaendelea kusema:
2 "Uwe na subira zaidi ninapoendelea kueleza,

Kwa maana bado nina maneno ya kusema kwa niaba ya Mungu.

- 3** Nitazungumza kwa kina kuhusu ninayojua, Nami nitatangaza kwamba uadilifu ni wa Muumba wangu.^c

- 4** Kwa kweli maneno yangu si ya uwongo; Yule ambaye ni mkamilifu katika ujuzi^d yuko hapa mbele yako.

- 5** Kwa kweli, Mungu ana nguvu,^e naye hamkatai yeyote; Yeye ni mkuu katika nguvu zake za uelewaji.*

- 6** Hatawaacha waovu wae-ndeleo kuishi,^f Lakini huwapa haki wanaoteseka.^g

- 7** Yeye haondoi macho yake kwa waadilifu;^h Huwaketisha kwenye viti vya ufalme pamoja na wafalme,^{*i} nao wana-kwezwa milele.

- 8** Lakini ikiwa wamefungwa kwa pingu Na kunaswa na kamba za mateso,

36:5 *Tnn., "moyo." 36:7 *Au labda, "Huwaketisha wafalme kwenye viti vya ufalme."

- 9** Huwafunulia mambo waliyotenda,
Uovu wao uliosababishwa na kiburi chao.
- 10** Hufungua masikio yao ili wapokee marekebisho
Na kuwaambia waache kutenda makosa.^a
- 11** Wakitii na kumtumikia,
Wataishi siku zao zote kwa ufanisi,
Na miaka yao itafurahi.^b
- 12** Lakini wasipatii, wataa-
ngamia kwa upanga*^c
Na kufa bila ujuzi.
- 13** Wanaomkataa Mungu*
moyoni watakuwa na kinyongo.
Hawalilii msaada hata anapowafunga.
- 14** Wanakufa wakiwa bado vijana,^d
Wakitumia* maisha yao miongoni mwa wanaume makahaba wa hekaluni.^e
- 15** Lakini Mungu huwaokoa wanaoteseka wakati wanapoteseka;
Hufungua sikio lao wanapokandamizwa.
- 16** Hukuvuta mbali kutoka kwenye ukingo wa taabu^f
Na kukuleta mahali penye nafasi kubwa, pasipo na vizuizi,^g
Na meza yako itakuwa na chakula chenye lishe ili kukufariji.^h
- 17** Kisha utaridhika na hukumu itakayowapata waovu,ⁱ
Hukumu itakapotolewa na haki kutetewa.

36:12 *Au "kwa silaha." **36:13** *Au "Waasi imani." **36:14** *Au labda, "Wakimaliza."

SURA YA 36

a Eze 18:30

b Yer 26:13

c Ayu 33:16-18
Isa 1:19, 20
Ro 2:8

d Zb 55:23

e 1Fa 14:24

f Isa 30:21

g Zb 18:19

h Isa 55:2

i Met 2:22
Yer 25:31

Safu ya 2

a Met 19:19
Met 29:22b Ayu 34:20
Zb 33:16
Met 11:4

c Ebr 11:24, 25

d Isa 40:14

e Ayu 34:10
Ro 9:14f Zb 92:5
Zb 104:24

g Kut 15:1

h Zb 145:3
Zb 148:13
Ufu 15:3i Zb 90:2
Zb 102:25-27
1Ti 1:17
Ebr 1:10-12j Mwa 2:6
Amo 5:8

- 18** Lakini jihadhari ghadhabu isikufanye uwe na chuki,^{*a}
Wala usikubali rushwa kubwa ikupotoshe.
- 19** Je, kilio chako cha kuomba msaada
Au mojawapo ya jitihada zako nyingi inaweza kukuepusha na taabu?^b
- 20** Usiutamani usiku,
Watu wanapotoweka kati ka makao yao.
- 21** Jihadhari usigeukie kute-
nda uovu,
Kuchagua uovu badala ya mateso.^c
- 22** Tazama! Mungu amekwezwa katika nguvu zake;
Ni nani aliye mfundishaji kama yeye?
- 23** Ni nani ameelekeza* njia yake^d
Au kumwambia, 'Jambo ulilotenda si sawa'?'^e
- 24** Kumbuka kuzitukuza kazi zake,^f
Ambazo wanadamu wameimba kuzihusu.^g
- 25** Wanadamu wote wameziona,
Mwanadamu anayeweza kufa huzitazama kutoka mbali.
- 26** Naam, Mungu ni mkuu kuliko tunavyoweza kujua;^h
Idadi ya miaka yake haiwezi kufahamika.^{*i}
- 27** Yeye huvuta juu matone ya maji;^j
Yanaganda na kuwa mvua kutokana na ukungu wake;

36:18 *Au "upige makofi kwa chuki."

36:23 *Au labda, "amechambua; amefanya awajibike kuhusu." **36:26** *Au "haichunguziki."

28 Kisha mawingu huyamwaga chini;^a
Yanawanyeshea wana-damu.

29 Kuna yeyote anayeweza kuelewa matabaka ya mawingu,
Mngurumo unaotoka kati-ka hema lake?^{*b}

30 Tazama jinsi anavyoita-ndaza radi^{*c} yake juu yake
Na kufunika vilindi vya[#] bahari.

31 Kwa vitu hivyo yeye huwa-tegemeza^{*} watu;
Huwapa chakula kwa wi-ngi.^d

32 Hufunika radi kwa mikono yake,
Naye huielekeza kwenye shabaha yake.^e

33 Mngurumo wake husimulia kumhusu,
Hata mifugo husema ni nani anayekuja.^{*}

37 “Kwa sababu hiyo moyo wangu hupigapiga
Na kuruka kutoka mahali pake.

2 Sikiliza kwa makini mri-ndimo wa sauti yake
Na mngurumo unaotoka kinywani mwake.

3 Huuachilia kwa ghafla chini ya mbingu zote
Na kuituma radi yake^f mpaka kwenye miisho ya dunia.

4 Kisha sauti ya mngurumo husikika;
Hunguruma kwa sauti yenye fahari,^g

36:29 *Tnn., “kibanda chake.” **36:30** *Tnn., “nuru.” **36:31** *Au labda, “huwatetea.” **36:33** *Au labda, “husema ni nini kinachokuja.”

SURA YA 36

a Met 3:20
Isa 55:10
Yer 14:22

b 2Sa 22:12

c Ayu 37:3

d Mdo 14:17

e 2Sa 22:15
Zb 18:14
Zb 144:6

SURA YA 37

f Ayu 37:11
Zb 97:4

g Ayu 40:9
Zb 29:3
Zb 68:33

Safu ya 2

a 2Sa 22:14

b Mhu 3:11
Ufu 15:3

c Zb 147:16

d Amo 9:6

e Zb 104:3

f Met 25:23

g Zb 147:16

h Ayu 38:29, 30

i Ayu 37:3

j Zb 148:8

k Kut 9:23
1Sa 12:17, 18

l Ifa 18:45
Ayu 36:29, 31
Ayu 38:25-27
Yak 5:17, 18

Naye haizuii radi sauti yake inaposikiwa.

5 Mungu hunguruma kwa sauti yake^a kwa njia inayostaajibisha;
Hufanya mambo makuu ambayo hatuwezi kuelewa.^b

6 Kwa maana huiambia the-luji, ‘Anguka duniani,’^c
Na mvua kubwa, ‘Nyesha kwa nguvu.’^d

7 Mungu husimamisha shughuli zote za wanadamu^{*}
Ili kila mwanadamu anayeweza kufa ajue kazi Yake.

8 Wanyama wa mwituni huingia katika mapango yao
Na kubaki katika makao yao.

9 Upepo wa dhoruba huvuma kutoka katika chumba chake,^e
Na baridi huletwa na pepo za kaskazini.^f

10 Kwa pumzi ya Mungu, barafu hutokea,^g
Na maji mengi huganda kabisa.^h

11 Naam, huyalemea mawingu kwa mvuke;
Hutawanya radi yakeⁱ mawinguni;

12 Huzunguka-zunguka anakoyaelekeza;
Hutekeleza chochote ana-choamuru/ juu ya dunia inayokaliwa.^{*}

13 Iwe ni adhabu^{*k} au kwa ajili ya nchi
Au kwa ajili ya upendo mshikamanifu, yeye husababisha yatendeke!^l

37:7 *Tnn., “huweka muhuri juu ya mko-no wa kila mwanadamu.” **37:12** *Au “ardhi inayozaa.” **37:13** *Tnn., “fimbo.”

- 14** Sikiliza hili, Ayubu;
Tulia na utafakari kwa
makini kazi za Mungu
zinazostaajabisha.^a
- 15** Je, unajua jinsi Mungu
anavyoongoza*
mawingu
Na jinsi anavyosababisha
radi imweke kutoka kati-
ka mawingu yake?
- 16** Je, unajua jinsi mawingu
yanavyoelea?^b
Hizi ni kazi zinazostaaja-
bisha za Yule ambaye ni
mkamilifu katika ujuzi.^c
- 17** Kwa nini mavazi yako ya-
napata joto
Wakati dunia imetulia kwa
sababu ya upepo wa
kusini?^d
- 18** Je, waweza, pamoja naye,
kuzitandaza* anga^e
Zilizo ngumu kama kioo
cha chuma?
- 19** Tuambie tunalopaswa
kumwambia;
Hatuwezi kumjibu kwa
sababu tuko gizani.
- 20** Je, anapaswa kuambiwa
kwamba ninataka kuzu-
ngumza?
Au kuna yeyote ambaye
amesema jambo ambalo
lazima ajulishwe?^f
- 21** Hata hawawezi kuona
nuru,*
Ingawa inang'aa angani,
Mpaka upepo unapopita
na kuondoa kabisa
mawingu.
- 22** Fahari inayong'aa kama
dhahabu hutoka kas-
kazini;
Utukufu wa Mungu^g unao-
gopesha.

37:15 *Au "anavyoamuru." 37:18

*Au "kuzikunjua." 37:21 *Yaani,
ya jua.

SURA YA 37

a Zb 111:2

Zb 145:5

b Ayu 36:29

c Ayu 36:4

Zb 18:30

Zb 104:24

d Lu 12:55

e Isa 44:24

f Ro 11:34

g 1Nya 16:27

Zb 8:1

Safu ya 2

a Zb 145:3

Mhu 3:11

Ro 11:33

b 1Nya 29:11

Ayu 36:22

Isa 40:26

c Kum 32:4

Zb 33:5

Zb 37:28

d Zb 11:7

Zb 71:19

e Zb 33:8

Met 1:7

Mt 10:28

f Met 3:7

Mt 11:25

Ro 11:20

Ro 12:16

1Ko 1:26

SURA YA 38

g Kut 19:16, 19

1Fa 19:11

h Ayu 42:3

i Mwa 1:1

Ne 9:6

Zb 136:6

Met 8:29

Ebr 1:10

j Zb 104:5

k Ufu 22:16

l Mwa 6:2

1Fa 22:19

Ayu 1:6

Ayu 2:1

Zb 89:6

m Zb 33:7

Met 8:29

- 23** Hatuwezi kumwelewa
Mweza-Yote;^a
Ana nguvu nyingi,^b
Na hapotoshi kamwe haki^c
na uadilifu wake
mwingi.^d
- 24** Kwa hiyo watu wanapaswa
kumwogopa.^e
Kwa sababu yeye hampe-
ndi yeyote anayefikiri
ana hekima.^f
- 38** Kisha Yehova akamjibu
Ayubu kutoka katika
dhoruba ya upepo.^g

- 2** "Ni nani huyu anayepoto-
sha mashauri yangu
Na kuzungumza bila
ujuzi?^h
- 3** Tafadhali, jitayarisha*
kama mwanamume;
Nitakuuliza maswali, nawe
unijibu.
- 4** Ulikuwa wapi nilipoweka
msingi ya dunia?ⁱ
Niambie, ikiwa unafikiri
unaelewa.
- 5** Ni nani aliyeweka vipimo
vyake, ikiwa unajua,
Au ni nani aliyenyoosha
kamba ya kupimia juu
yake?
- 6** Nguzo zake zilizamishwa
ndani ya nini,
Au ni nani aliyeweka jiwe
lake la pembeni,^j
- 7** Nyota za asubuhi^k zilipo-
paza kelele pamoja kwa
shangwe,
Na wana wote wa Mungu*^l
wakaanza kushangilia
kwa sauti?
- 8** Na ni nani aliyezuia baha-
ri nyuma ya milango^m
Ilipotoka kwa nguvu kati-
ka tumbo la uzazi,

38:3 *Tnn., "jifunge." 38:7 *Msemu wa
Kiebrania unaorejelea malaika, wana wa
Mungu.

- 9** Nilipoivalisha mawingu
Na kuifunika kwa* giza
zito,
- 10** Nilipoiwekea mpaka
wangu
Na kuweka makomeo yake
na milango yake mahali
pake,^a
- 11** Nami nikaiambia, 'Unawe-
za kufika hapa, lakini
usipite hapa;
Hapa ndipo mawimbi yako
ya kifahari yatakapoko-
mea'?^b
- 12** Je, umewahi kuiamuru*
asubuhi
Au kuyafanya mapamba-
zuko yajue mahali pake,^c
- 13** Ili yaenee mpaka kwenye
miisho ya dunia
Na kuwakung'uta waovu
kutoka humo?^d
- 14** Dunia hubadilika kama
udongo wa mfinyanzi
utiwapo muhuri,
Na vitu vilivyomo hung'aa
kama mapambo ya vazi.
- 15** Lakini waovu hunyimwa
nuru yao,
Na mkono wao ulioinuliwa
huvunjwa.
- 16** Je, umeshuka chini kwe-
nye chemchemi za
bahari
Au kuchunguza vilindi vya
maji?^e
- 17** Je, umeonyeshwa mala-
ngo ya kifo,^f
Au umeona malango ya
giza zito?^{*g}
- 18** Je, umelewa upana mku-
bwa sana wa dunia?^h
Niambie, ikiwa unajua
haya yote.

38:9 *Au "kuifungafunga katika."
38:12 *Tnn., "Je, katika siku zako umeia-
muru." **38:17** *Au "kivuli cha kifo."

SURA YA 38

a Mwa 1:9
Yer 5:22

b Met 8:29

c Mwa 1:5
Zb 74:16

d Ayu 24:15
1Th 5:7

e Mwa 1:2
Zb 77:19

f Zb 9:13
Mt 16:18

g Ayu 10:21, 22

h Zb 74:17
Zb 89:11

Safu ya 2

a Isa 45:7

b Ayu 37:6

c Yos 10:11
Isa 30:30

d Kut 9:24
Eze 13:13

e Zb 135:7

f Ayu 28:26

g Zb 104:13
Zb 107:35

h Zb 147:7, 8

i 1Sa 12:18
Isa 30:23
Yer 5:24

j Mwa 27:28

- 19** Nuru hukaa upande gani?^a
Na makao ya giza yako
wapi,
- 20** Ili ulipeleke katika eneo
lake
Na kuelewa vijia vinavyoe-
lekea nyumbani kwake?
- 21** Je, unajua hayo kwa
sababu ulikuwa tayari
umezaliwa
Na idadi ya miaka yako ni
mingi?*
- 22** Je, umeingia kwenye
maghala ya theluji,^b
Au umeyaona maghala ya
mvua ya mawe,^c
- 23** Ambayo nimeyahifadhi
kwa ajili ya wakati wa
taabu,
Kwa ajili ya siku ya mapi-
gano na vita?^d
- 24** Nuru* hutawanywa kuto-
ka upande gani,
Na upepo wa mashariki
huvuma duniani kutoka
wapi?^e
- 25** Ni nani amechimba mtaro
kwa ajili ya mafuriko
Na kutengeneza kijia kwa
ajili ya mawingu ya dho-
ruba yenye ngurumo,^f
- 26** Na kuifanya mvua inyeshe
mahali ambapo watu
hawaishi,
Nyikani ambako hakuna
wanadamu,^g
- 27** Ili kutosheleza maeneo
yaliyoharibiwa yenye
ukiwa
Na kufanya majani yachi-
puke?^h
- 28** Je, mvua ina baba,ⁱ
Au ni nani baba ya matone
ya umande?/
- 29** Barafu ilitoka kwenye
tumbo la uzazi la nani,

38:21 *Tnn., "Na idadi ya siku zako ni
nyingi?" **38:24** *Au labda, "Radi."

- Na ni nani aliyeezaa theluji ya mbinguni^a
- 30** Maji yanapofunikwa kana kwamba na jiwe, Na sehemu ya juu ya vili-ndi vya maji inapoganda kabisa?^b
- 31** Je, unaweza kufunga kamba za kundi la nyota la Kima*
Au kufungua kamba za kundi la nyota la Kesili?^{#c}
- 32** Je, unaweza kuliongoza nje kundi la nyota* kati-ka majira yake
Au kulielekeza kundi la nyota la Ashi# pamoja na wanawe?
- 33** Je, unajua sheria zinazoo-ngoza mbingu,^d
Au unaweza kutumia mamlaka ya sheria hizo* duniani?
- 34** Je, unaweza kuinua sauti yako mpaka mawinguni Ili kusababisha mafuriko ya maji yakufunike?^e
- 35** Je, unaweza kuutuma umeme wa radi?
Je, utakuja na kukwambia, 'Niko hapal!'
- 36** Ni nani aliyeweka hekima mawinguni*^f
Au kuyapa ulelawaji matu- kio ya angani?^{#g}
- 37** Ni nani aliye na hekima ya kutosha kuhesabu mawi- ngu,

38:31 *Labda ni nyota zinazoitwa Pleiadesi katika kundi la nyota la Taurusi, au Ng'ombe. #Labda ni kundi la nyota la Oriani. **38:32** *Tnn., "Mazarothi." Kwenye 2Fa 23:5, neno linalohusiana na hilo ambalo liko katika wingi linarejelea makundi ya nyota za unajimu. #Labda ni kundi la nyota la Dubu Mku-bwa (Kundi Kubwa la Ursa). **38:33** *Au labda, "mamlaka Yake." **38:36** *Au labda, "ndani ya mwanadamu." #Au labda, "kuweka ulelawaji akilini."

SURA YA 38

a Zb 147:16

b Ayu 37:10

c Amo 5:8

d Met 3:19
Yer 31:35
Yer 33:25

e Zek 10:1

f Yer 10:12

g Zb 136:5
Met 3:20

Safu ya 2

a Yer 10:13

b Zb 104:21
Zb 145:15, 16
Nah 2:12c Zb 147:9
Mt 6:26
Lu 12:24

SURA YA 39

d Zb 104:18

e Zb 29:9

f Ayu 24:5
Zb 104:10, 11

- Au ni nani anayeweza kuinamisha mitungi ya maji ya mbinguni^a
- 38** Mavumbi yanapomiminika na kugandamana
Na mabonge ya udongo yanaposhikamana?
- 39** Je, unaweza kumwindia simba mawindia
Au kutosheleza hamu ya chakula ya wanasimba^b
- 40** Wanapojikunyata katika maficho yao
Au wanaponyemelea ma-pangoni mwao?
- 41** Ni nani anayemtayarishia chakula kunguru^c
Makinda wake wanapo-mlilia Mungu wakiomba msaada
Na kutangatanga kwa sababu hawana chakula?
- 39** "Je, unajua mbuzi wa milimani huzaa wakati gani?^d
Je, umewahi kuwatazama paa wakizaa watoto wao?^e
- 2** Je, wewe huhesabu miezi ambayo wanabeba mi- mba?
Je, unajua wakati wanapo- zaa?
- 3** Wao huchuchumaa wana- pozaa watoto wao,
Na uchungu wao wa kuzaa huisha.
- 4** Watoto wao hupata nguvu na kukua mbugani;
Huenda zao na hawarudi.
- 5** Ni nani aliyemwacha huru punda mwitu,^f
Na ni nani aliyemfungua kamba punda mwitu?
- 6** Nimelifanya jangwa ta- mbarara kuwa makao yake

- Na nchi yenye chumvi kuwa makazi yake.
- 7** Yeye hudharau vurugu za mji; Hasikii kelele za mtu anayemwongoza.
- 8** Hutangatanga milimani, akitafuta malisho, Akitafuta mmea wowote wa kijani.
- 9** Je, fahali mwigu yuko tayari kukutumikia?^a Je, atalala zizini mwako* usiku?
- 10** Je, utamfunga fahali mwigu kwa kamba ili alime, Au, je, atakufuata ili alime* bondeni?
- 11** Je, utazitumaini nguvu zake nyingi Na kumwacha afanye kazi zako ngumu?
- 12** Je, utamtegemea akuletee mavuno yako,* Na je, atayakusanya kwenye uwanja wako wa kupuria?
- 13** Mabawa ya mbuni hupigapiga kwa shangwe, Lakini, je, mabawa na manyoya yake yanaweza kulinganishwa na ya korongo?^b
- 14** Kwa maana yeye huacha mayai yake ardhini, Na kuyapasha joto mavumbini.
- 15** Yeye husahau kwamba mguu fulani unaweza kuyavunja Au kwamba mnyama wa mwigu anaweza kuyakanyaga.
- 16** Huwatendea wanawe kwa

39:9 *Au "katika hori lako." 39:10 *Au "alime matuta." 39:12 *Tnn., "mbegu zako."

SURA YA 39

a Kum 33:17

b Zb 104:17
Zek 5:9

Safu ya 2

a Omb 4:3

b Zb 147:10
Isa 31:1

c Yer 8:16

d Amu 5:22
Zb 32:9e Met 21:31
Yer 46:9
Yer 47:3
Hab 1:8f Isa 5:28
Yer 8:6

g Yer 46:4

ukatili, kana kwamba si wake;^a

Haogopi kwamba huenda kazi yake ngumu ikawa ya bure.

- 17** Kwa maana Mungu amemnyima* hekima Naye hajamgawia uelewaji.
- 18** Lakini anapoinuka na kupigapiga mabawa yake, Humcheka farasi na yule aliyempanda.
- 19** Je, ni wewe unayempa farasi nguvu zake?^b Je, unamvika shingoni manyoya marefu yanayotikisika?
- 20** Je, unaweza kumfanya aruke kama nzige? Mkoromo wake wa mari-ngo unatisha.^c
- 21** Yeye hukwangua ardhi bondeni na kushangilia kwa nguvu;^d Hukimbia kwenda vitani.*^e
- 22** Huicheka hofu na haogopi chochote.^f Harudi nyuma kwa sababu ya upanga.
- 23** Podo la mishale hutoa sauti kando yake, Mkuki na fumo humetameta.
- 24** Husonga mbele* huku akitetemeka kwa msisimko, Hawezi kusimama tuli anaposikia^g mlio wa pembe.
- 25** Pembe inapolia, husema, 'Aha!' Hunusa vita kutoka mbali sana Na kusikia kelele za makamanda na kelele za vita.^g

39:17 *Tnn., "amemfanya asahau." 39:21 *Tnn., "Huenda kukutana na silaha." 39:24 *Tnn., "Humeza ardhi (dunia)." *Au labda, "Haamini."

- 26** Je, ni kwa uelewaji wako kwamba kipanga huruka,
Akiyatandaza mabawa yake kuelekea kusini?
- 27** Au, je, ni kwa agizo lako kwamba tai hupaa juu?^a
Na kujenga kiota chake juu sana,^b
- 28** Na kulala usiku kucha juu ya jabali,
Akiishi kwenye ngome yake juu ya mwamba uliochongoka?*
- 29** Akiwa hapo yeye hutafuta chakula;^c
Macho yake hutazama mbali sana.
- 30** Makinda yake hufyonza damu;
Na penye mzoga, ndipo alipo.”^d
- 40** Yehova akaendelea kumjibu Ayubu:
- 2** “Je, mtu anayetafuta makosa anapaswa kushindana na Mweza-Yote?^e
Acha yule anayetaka kumkaripia Mungu ajibu.”^f
- 3** Ayubu akamjibu Yehova:
- 4** “Tazama! Mimi sistahili.^g
Nitakujibu nini?
Ninafunika kinywa changu kwa mkono.^h
- 5** Niliongea mara moja, lakini sitajibu tena;
Mara mbili, lakini sitaongea tena.”
- 6** Kisha Yehova akamjibu Ayubu kutoka katika dhoruba ya upepo:ⁱ
- 7** “Tafadhali, jitayarisha* kama mwanamume;
Nitakuuliza maswali, nawe unijibu.^j

39:28 *Tnn., “kwenye jino la jabali.”
40:7 *Tnn., “jifunge.”

SURA YA 39

a Met 23:5
Isa 40:31

b Yer 49:16
Oba 4

c Ayu 9:26
Yer 49:22

d Mt 24:28

SURA YA 40

e Ayu 33:12, 13
Isa 45:9

f Ayu 13:3
Ayu 23:3-5
Ayu 31:35

g Ayu 42:5, 6

h Zb 39:9
Met 30:32

i Ayu 38:1

j Ayu 38:3
Ayu 42:4

Safu ya 2

a Zb 51:4
Ro 3:4

b Kut 15:6
Zb 89:13
Isa 40:26
1Ko 10:22

c Ayu 37:4
Zb 29:3

- 8** Je, utatilia shaka* haki yangu?
Je, utanishutumumu ili uwe mwadilifu?^a
- 9** Je, una mkono wenye nguvu kama mkono wa Mungu wa kweli,^b
Au je, sauti yako inaweza kunguruma kama yake?^c
- 10** Tafadhali, jipambe kwa utukufu na ukuu;
Jivike heshima na fahari.
- 11** Mwaga ghadhabu ya hasira yako;
Mtazame kila mwenye kiburi, umshushe chini.
- 12** Mtazame kila mwenye kiburi, umnyenyekeze,
Na uwakanyage waovu mahali wanaposimama.
- 13** Wafiche wote mavumbini;
Wafunge* mahali palipofichika,
- 14** Ndipo hata mimi nitakapokiri mbele yako*
Kwamba mkono wako wa kulia unaweza kukuo-koa.
- 15** Tazama, huyu ni Behemothi* niliyemuumba kama nilivyokuumba.
Yeye hula majani kama ng'ombe dume.
- 16** Tazama nguvu zilizo kiunoni mwake
Na nguvu zilizo katika misuli ya tumbo lake!
- 17** Huukaza mkia wake kama mwerezi;
Kano za mapaja yake zimefumwa pamoja.
- 18** Mifupa yake ni mabomba ya shaba;

40:8 *Au “utabatilisha.” 40:13 *Tnn., “Zifunge nyuso zao.” 40:14 *Au “nitakapokupongeza.” 40:15 *Labda ni kiboko.

Miguu yake ni kama fito za chuma kilichofuliwa.

19 Yeye ni wa kwanza miongoni mwa kazi za Mungu;

Ni Muumba wake tu anayeweza kumkaribia kwa upanga wake.

20 Kwa maana milima huza-lisha chakula kwa ajili yake,

Ambako wanyama wote wa mwituni huचेza.

21 Hulala chini ya miti ya miyungiyungi,

Kwenye kivuli cha matete mahali penye umajimaji.

22 Miti ya miyungiyungi humfunika kwa kivuli, Na mierebi ya bondeni* humzunguka.

23 Mto anaposukasuka, yeye hashtuki.

Haogopi hata maji ya Yordani^a yakifurika kinywani mwake.

24 Je, kuna yeyote anayeweza kumkamata akiwa macho,

Au kumtoboia pua kwa kulabu?*

41 "Je, unaweza kumvua Lewiathani*^b kwa ndoano

Au kuufunga chini ulimi wake kwa kamba?

2 Je, unaweza kupitisha kamba* kwenye mianzi ya pua yake

Au kutoboa mataya yake kwa kulabu?*

3 Je, atakusihhi sana umhurumie,

Au je, atazungumza nawe kwa upole?

40:22 *Au "korongoni." 40:24 *Tnn., "mtego." 41:1 *Labda ni mamba. 41:2 *Tnn., "unyasi." *Tnn., "mwiba."

SURA YA 40

a Yos 3:15

SURA YA 41

b Zb 104:25, 26

Safu ya 2

a Ayu 41:26

b 2Nya 20:6

Da 4:35

Mdo 11:17

Ro 9:19

c Ro 11:35

d Kum 10:14

Zb 24:1

Zb 50:12

1Ko 10:26

4 Je, atafanya agano pamoja nawe,

Ili umfanye awe mtumwa wako milele?

5 Je, utamchezea kama ndege

Au kumfanga kamba kwa ajili ya wasichana wako?

6 Je, wafanyabiashara watamtumia kubadilishana bidhaa?

Je, watamgawanya miongoni mwao?

7 Je, utaijaza ngozi yake mikuki^a

Au kichwa chake mikuki ya kuvulia samaki?

8 Mguse kwa mkono wako; Utakumbuka vita hivyo na kamwe hutarudia kufanya hivyo!

9 Ni kazi bure kujaribu kumtiisha.

Ukimwona tu utashtuka.*

10 Hakuna anayethubutu kumchokoza.

Basi ni nani anayeweza kukabiliiana nami?^b

11 Ni nani aliyenipa kitu chochote kwanza ili nimilipe?^c

Chochote kilicho chini ya mbingu ni changu.^d

12 Sitakaa kimya kuhusu miguu yake,

Kuhusu nguvu zake na mwili wake wenye umbo zuri.

13 Ni nani aliyemvua vazi lake la nje?

Ni nani atakayeingia katikati ya mataya yake yaliyo wazi?

14 Ni nani anayeweza kuifungua kwa nguvu milango ya kinywa chake?*

41:9 *Au "utaanguka chini." 41:14 *Tnn., "uso wake."

Meno yake kuzunguka
kinywa chote yanatisha.

15 Mgongo wake una safu za
magamba*

Yaliyoshikamana kabisa
pamoja.

16 Kila gamba limeshikama-
na kabisa na lingine

Hivi kwamba hewa haiwezi
kupenya katikati ya
magamba hayo.

17 Yamefungamana pamoja;
Yameshikamana na haya-
wezi kutenganishwa.

18 Mkoromo wake hufanya
nuru imweke,

Na macho yake ni kama
miale ya mapambazuko.

19 Mimweko ya radi hutoka
kinywani mwake;

Cheche za moto huruka
nje.

20 Moshi hufuka kutoka kati-
ka mianzi ya pua yake,
Kama tanuru linalowaka
moto wa matete.

21 Pumzi yake huwasha
makaa ya mawe,
Na mwali wa moto huruka
kutoka kinywani mwake.

22 Shingo yake ina nguvu
nyingi,
Wanaokutana naye huki-
mbia kwa hofu.

23 Mikunjo ya ngozi yake
imeunganishwa kabisa
pamoja;
Ni imara, kana kwamba
imetengenezwa kwa chu-
ma, nayo haiwezi
kutikisika.

24 Moyo wake ni mgumu
kama jiwe,
Naam, ni mgumu kama
jiwe la chini la kusagia.

41:15 *Au labda, "Anajivunia safu zake
za magamba."

Safu ya 2

SURA YA 41

a Ayu 41:7

25 Anapoinuka, hata mashu-
jaa huogopa;

Mshindo wake huwababai-
sha.

26 Hakuna upanga unaomfi-
kia unaoweza kushinda;
Wala mkuki, mshale, au
ncha ya mshale.^a

27 Yeye huona chuma kama
nyasi,
Shaba kama ubao uliooza.

28 Mshale haumfanyi aki-
mbie;
Mawe ya kombeo huwa
kama nyasi kavu kwenye
mwili wake.

29 Yeye huona rungu kuwa
kama nyasi kavu,
Naye huucheka mvumo wa
mkuki.

30 Chini, yeye ni kama vigae
vyenye ncha kali;
Hujinyoosha kwenye
matope kama kifaa
cha kupuria.^b

31 Hufanya vilindi vichemke
kama chungu;
Huikoroga bahari kama
chungu cha manukato.

32 Anapopita huacha njia
ikimetameta.
Mtu anaweza kudhani
kwamba vilindi vina mvi.

33 Hakuna chochote kilicho
kama yeye duniani,
Kiumbe aliyeumbwa asio-
gope.

34 Hukodolea macho cho-
chote chenye kiburi.
Yeye ni mfalme wa wa-
nyama wote wa mwituni
wenye fahari."

42 Kisha Ayubu akamjibu
Yehova:

2 "Sasa ninajua kwamba
unaweza kufanya
mambo yote

b Isa 41:15

Na kwamba hakuna jambo lolote unalokusudia lisi-lowezekana kwako.^a

3 Ulisema, 'Ni nani huyu anayepotosha mashauri yangu bila ujuzi?'^b

Kwa hiyo nikazungumza, lakini sikuwa na uelewaji Kuhusu mambo yanayonistaajabisha sana, ambayo siyajui.^c

4 Ulisema, 'Tafadhali sikiliza, nami nitaongea. Nitakuuliza maswali, nawe unijibu.'^d

5 Masikio yangu yamesikia habari zako, Lakini sasa ninakuona kwa macho yangu.

6 Ndiyo sababu ninabatilisha* niliyosema,^e Nami ninatubu katika mavumbi na majivu."^f

7 Baada ya Yehova kumwambia Ayubu maneno hayo, Yehova akamwambia Elifazi Mtemani:

"Hasira yangu inawaka dhidi yako na rafiki zako wawili,^g kwa sababu hamkusema ukweli kunihusu^h kama alivyofanya mtumishi wangu Ayubu.

8 Sasa chukueni ng'ombe dume saba na kondoo dume saba kisha mwende kwa mtumishi wangu Ayubu, na mtoe dhabihu ya kuteketezwa kwa ajili yenu. Na mtumishi wangu Ayubu atasali kwa ajili yenu.ⁱ Kwa hakika nitakubali ombi lake* nami sitawate ndea kulingana na upumbavu wenu, kwa sababu hamkusema ukweli kunihusu kama alivyofanya mtumishi wangu Ayubu."

9 Kwa hiyo Elifazi Mtemani,

42:6 *Au "ninafuta." 42:8 *Tnn., "Kwa hakika nitauinua uso wake."

SURA YA 42

a Mwa 18:14
Zb 135:6
Isa 43:13
Isa 55:10, 11
Yer 32:17
Mk 10:27
Lu 18:27

b Ayu 38:2

c Zb 40:5
Zb 139:6

d Ayu 38:3
Ayu 40:7

e Ayu 40:4

f Ezr 9:6
Zb 51:17

g Ayu 2:11

h Ayu 11:6
Ayu 15:14, 15
Ayu 22:2, 3

i Mwia 20:17
Yak 5:15

Safu ya 2

a Mt 6:14

b Ayu 2:6, 7
Yak 5:11

c Mwa 32:10
1Sa 2:7
2Nya 25:9
Met 22:4
Isa 61:7

d Ayu 19:13

e Met 3:33
Met 10:22
Ebr 11:6
Yak 5:11

f Ayu 1:3

g Ayu 1:1, 2

Bildadi Mshua, na Sofari Mnaamathi wakaenda na kufanya kama Yehova alivyowaaambia. Kisha Yehova akakubali sala ya Ayubu.

10 Baada ya Ayubu kusali kwa ajili ya rafiki zake,^a Yehova akamwondolea Ayubu dhiki^b na kumrudishia ufanisi wake.* Yehova akampa maradufu ya vitu alivyokuwa navyo awali.^c **11** Ndugu na dada zake wote pamoja na rafiki zake wote wa zamani^d waka-ja kwake na kula pamoja naye nyumbani mwake. Wakampa pole na kumfariji kwa sababu ya mateso yote ambayo Yehova alikuwa ameruhusu yampate. Kila mmoja wao akampa kipande cha fedha na pete ya dhahabu.

12 Kwa hiyo, Yehova alibariki sehemu ya mwisho ya maisha ya Ayubu kuliko ya kwanza,^e na Ayubu akawa na kondoo 14,000, ngamia 6,000, ng'ombe 2,000,* na punda jike 1,000.^f **13** Akapata pia wana wengine saba na mabinti wengine watatu.^g **14** Akamwita binti yake wa kwanza Yemi-ma, wa pili Kezia, na wa tatu Kereni-hapuku. **15** Katika nchi yote hapakuwa na wanawake warembo kama mabinti wa Ayubu, na baba yao aliwapa urithi pamoja na ndugu zao.

16 Baada ya hayo Ayubu aliishi miaka 140, akawaona watoto wake na wajukuu wake—vizazi vinne. **17** Mwishowe Ayubu akafa, baada ya kuishi maisha marefu na yenye kuridhisha.*

42:10 *Tnn., "Yehova akaondoa utekwa wa Ayubu." 42:12 *Yaani, jozi 1,000 za ng'ombe. 42:17 *Tnn., "akiwa amezee-ka na akiwa amejaa siku."

ZABURI

YALIYOMO

- 1 Njia mbili zatofautishwa
Kusoma sheria ya Mungu huleta furaha (2)
Waadilifu ni kama mti unaozaa matunda kwa wingi (3)
Wavuu ni kama makapi yanayopeperushwa mbali (4)
- 2 Yehova na mtiwa-mafuta wake
Yehova anayacheka mataifa (4)
Yehova amweka mfalme wake (6)
Mheshimuni mwana (12)
- 3 Kumtumaini Mungu licha ya hatari
'Kwa nini maadui wamekuwa wengi sana?' (1)
'Wokovu ni wa Yehova' (8)
- 4 Sala ya kumtumaini Mungu
'Kasirika, lakini usitende dhambi' (4)
'Nitalala usingizi kwa amani' (8)
- 5 Yehova ni kimbilio la mwadilifu
Mungu anachukua uovu (4, 5)
'Niongoze katika uadilifu wako' (8)
- 6 Ombi la kupata kibali
Waliokufa hawamsifu Mungu (5)
Mungu husikia sala za kuomba kibali (9)
- 7 Yehova ni Mwanuzi mwadilifu
'Nihukumu, Ee Yehova' (8)
- 8 Utukufu wa Mungu na heshima ya mwanadamu
'Jinsi jina lako lilivyo kuu!' (1, 9)
'Mwanadamu anayeweza kufa ana faida gani?' (4)
Mwanadamu avikwa taji la fahari (5)
- 9 Kutangaza kazi za Mungu zinazostaajibisha
Yehova ni kimbilio salama (9)
Kulijua jina la Mungu humaanisha kumtumaini yeye (10)
- 10 Yehova ni msaidizi wa wasio na uwezo
Mwovu hujigamba: "Hakuna Mungu" (4)
Wasio na uwezo humgeukia Yehova (14)
'Yehova ni Mfalme milele' (16)
- 11 Kumkimbilia Yehova
'Yehova yumo katika hekalu lake takatifu' (4)
Mungu humchukia yeyote anayependa ukatili (5)
- 12 Yehova ainuka ili kutenda
Maneno ya Mungu ni safi (6)
- 13 Kutamani wokovu wa Yehova
'Mpaka lini, Ee Yehova?' (1, 2)
Yehova huthawabisha kwelikweli (6)
- 14 Ufafanuzi kumhusu mpumbavu
'Hakuna Yehova' (1)
'Hakuna yeyote anayetenda mema' (3)
- 15 Ni nani anayeweza kuwa mgeni katika hema la Yehova?
Husema ukweli moyoni mwake (2)
Hachongeji (3)
Hutumiza ahadi hata inapomletea madhara (4)
- 16 Yehova ni Chanzo cha wema
'Yehova ni fungu langu' (5)
'Mawazo yangu hunirekebisha usiku' (7)
'Yehova yuko mkono wangu wa kulia' (8)
'Hutaniacha Kaburini' (10)
- 17 Sala ya kuomba ulinzi
'Umeuchunguza moyo wangu' (3)
'Katika kivuli cha mabawa yako' (8)
- 18 Kumsifu Mungu kwa sababu ya wokovu
'Yehova ni jabali langu' (2)
Yehova ni mshikamanifu kwa walio washikamanifu (25)
Njia ya Mungu ni kamilifu (30)
'Unyenyekevu wako hunifanya niwe mkuu' (35)
- 19 Umbaji wa Mungu na sheria yake hutoa ushahidi
'Mbingu hutangaza utukufu wa Mungu' (1)
Sheria kamilifu ya Mungu hurudisha nguvu (7)
'Dhambi nisizojuu' (12)
- 20 Wokovu kwa ajili ya mfalme mtiwa-mafuta wa Mungu

- Wengine hutegemea magari ya vita na farasi, "lakini sisi tunaliitia jina la Yehova" (7)
- 21 Baraka kwa mfalme anayemtumaini Yehova
Mfalme apewa maisha marefu (4)
Maadui wa Mungu watashindwa (8-12)
- 22 Baada ya kukata tamaa, amsifu Mungu
"Mungu wangu, kwa nini umeniacha?" (1)
"Wanalipigia kura vazi langu" (18)
Kumsifu Mungu kutanikoni (22, 25)
Dunia yote itamwabudu Mungu (27)
- 23 "Yehova ni Mchungaji wangu"
"Sitakosa chochote" (1)
"Huniburudisha" (3)
"Kikombe changu kimejazwa vizuri" (5)
- 24 Mfalme mtukufu aingia malangoni
'Dunia ni ya Yehova' (1)
- 25 Sala ya kuomba mwongozo na msamaha
"Nifundishe vijia vyako" (4)
"Urafiki wa karibu pamoja na Yehova" (14)
"Unisamehe dhambi zangu zote" (18)
- 26 Kutembea katika utimilifu
"Nichunguze, Ee Yehova" (2)
Kuepuka marafiki wabaya (4, 5)
'Nitapiga mwendo kuzunguka madhabahu ya Mungu' (6)
- 27 Yehova ni ngome ya uhai wangu
Kulithamini hekalu la Mungu (4)
Yehova anajali hata ikiwa wazazi hawajali (10)
"Mtumaini Yehova" (14)
- 28 Sala ya mtunga zaburi yasikiwa
'Yehova ni nguvu zangu na ngao yangu' (7)
- 29 Sauti ya Yehova yenye nguvu
Abuduni katika mapambo matakatifu (2)
"Mungu mtukufu hunguruma" (3)
Yehova huwapa nguvu watu wake (11)
- 30 Maombolezo yabadilishwa kuwa shangwe
Kibali cha Mungu hudumu maisha yote (5)
- 31 Kumkimbilia Yehova
- "Naiweka roho yangu mkononi mwako" (5)
"Yehova, Mungu wa ukweli" (5)
Wema mwingi wa Mungu (19)
- 32 Wenye furaha ni wale waliosamehewa
"Nikaungama dhambi yangu kwako" (5)
Mungu hukupa ufahamu (8)
- 33 Sifa kwa Muumba
"Mwimbieni wimbo mpya" (3)
Yehova aumba kupitia neno lake na roho yake (6)
Taifa la Yehova lina furaha (12)
Jicho la Yehova hulinda (18)
- 34 Yehova huwaokoa watumishi wake
"Na tulikweze jina lake pamoja" (3)
Malaika wa Yehova hulinda (7)
"Onjeni mwone kwamba Yehova ni mwema" (8)
'Hakuna hata mfupa wake mmoja uliovunjwa' (20)
- 35 Sala ya kuomba ukombozi kutoka kwa maadui
Maadui watafukuzwa (5)
Kumsifu Mungu katikati ya umati wa watu (18)
Achukiwa bila sababu (19)
- 36 Upendo mshikamanifu wa Mungu wenye thamani
Mwovu hamwogopi Mungu (1)
Mungu ni chanzo cha uhai (9)
"Kwa nuru yako tunaweza kuona nuru" (9)
- 37 Wanaomtumaini Yehova watafanikiwa
Usikasirishwe na waovu (1)
"Pata furaha tele katika Yehova" (4)
"Mkabidhi Yehova njia yako" (5)
"Wapole wataimiliki dunia" (11)
Waadilifu hawatakosa chakula (25)
Waadilifu wataishi milele duniani (29)
- 38 Sala ya mtu aliyetubu anayeteseka
"Nimesononeka na kushuka moyo kupita kiasi" (6)
Yehova huwasikia wale wanaomngojea (15)
"Nilihangaishwa na dhambi yangu" (18)
- 39 Ufupi wa maisha
Mwanadamu ni pumzi tu (5, 11)
"Usipuuze machozi yangu" (12)

- 40 Kumshukuru Mungu asiyeweze kulinganishwa na yeyote
Kazi za Mungu ni nyingi sana zisiweze kusimuliwa (5)
Dhabihu si jambo kuu kwa Mungu (6)
"Ninafurahia kufanya mapenzi yako" (8)
- 41 Sala katika kitanda cha ugonjwa
Mungu huwategemeza wagonjwa (3)
Asalitiwa na rafiki wa karibu (9)
- 42 Kumsifu Mungu akiwa Mwokozi Mtukufu
Kuwa na kiu kwa ajili ya Mungu kama paa aliye na kiu ya maji (1, 2)
"Kwa nini nimesononeka?" (5, 11)
"Mngojee Mungu" (5, 11)
- 43 Mungu ambaye ni Mwamuzi huokoa
"Itume nuru yako na kweli yako" (3)
"Kwa nini nimesononeka?" (5)
"Mngojee Mungu" (5)
- 44 Sala ya kuomba msaada
"Ni weve uliyetuokoa" (7)
Kama "kondoo wa kuchinjwa" (22)
"Amka utusaidie!" (26)
- 45 Ndoa ya mfalme mtiwa-mafuta
Maneno yenye fadhili (2)
"Mungu ni kiti chako cha ufalme milele" (6)
Mfalme anautamani urembo wa bibi harusi (11)
Wana watakuwa wakuu katika dunia yote (16)
- 46 "Mungu ni kimbilio letu"
Kazi za Mungu zinazostaajibisha (8)
Mungu akomesha vita katika dunia yote (9)
- 47 Mungu ni Mfalme wa dunia yote
'Yehova ni mwenye kuogopesha' (2)
Mwimbieni Mungu sifa (6, 7)
- 48 Sayuni, jiji la Mfalme Mtukufu
Shangwe ya dunia yote (2)
Likagueni jiji na minara yake (11-13)
- 49 Upumbavu wa kuutumaini utajiri
Hakuna mwanadamu anayeweze kumkomboa mwingine (7, 8)
Mungu hukomboa kutoka Kaburini (15)
Utajiri hauwezi kuokoa kutoka katika kifo (16, 17)
- 50 Mungu huhukumu kati ya mtu mshikamanifu na mwovu
Wanaofanya agano pamoja na Mungu kwa dhabihu (5)
"Mungu mwenyewe ni Mwamuzi" (6)
Wanyama wote ni wa Mungu (10, 11)
Mungu awafichua waovu (16-21)
- 51 Sala ya mtu aliyetubu
Mwenye dhambi tangu alipochukuliwa mimba (5)
"Nisafishe kutoka katika dhambi yangu" (7)
"Umba moyo safi ndani yangu" (10)
Moyo uliopondeka humpendeza Mungu (17)
- 52 Kuutumaini upendo mshikamanifu wa Mungu
Wanaojigamba kwa sababu ya uovu waonywa (1-5)
Wasiomwogopa Mungu wanautumaini utajiri (7)
- 53 Ufafanuzi kumhusu mpumbavu
"Hakuna Yehova" (1)
"Hakuna yeyote anayetenda mema" (3)
- 54 Sala ya kuomba msaada unapokuwa kati ya maadui
"Mungu ni msaidizi wangu" (4)
- 55 Sala ya mtu aliyesalitiwa na rafiki
Adhikiwa na rafiki wa karibu (12-14)
"Mtupie Yehova mzigo wako" (22)
- 56 Sala ya mtu anayeteswa
"Katika Mungu ninaweka tumaini langu" (4)
"Machizi yangu katika kiriba chako cha ngozi" (8)
"Mwanadamu ambaye ni duni tu atanifanya nini?" (4, 11)
- 57 Sala ya kuomba kibali
Kimbilio chini ya mabawa ya Mungu (1)
Maadui waanguka katika mtego wao wenyewe (6)
- 58 Kuna Mungu anayehukumu dunia
Sala ya kuomba waovu waadhibiwe (6-8)
- 59 Mungu ni ngao na kimbilio
"Usiwaonyeshe rehema wasaliti" (5)
"Nitaimba kuhusu nguvu zako" (16)
- 60 Mungu huwatiisha maadui
Wokovu kutoka kwa wanadamu hauna faida yoyote (11)

- "Kwa msaada wa Mungu tutapata nguvu" (12)
- 61 Mungu ni mnara wenye nguvu dhidi ya maadui
"Nitakuwa mgeni katika hema lako" (4)
- 62 Wokovu wa kweli hutoka kwa Mungu
"Ninamgojea Mungu kimyakimya" (1, 5)
'Mwageni mioyo yenu mbele za Mungu' (8)
Wanadamu ni pumzi tu (9)
Usitumaini mali (10)
- 63 Kumtamani Mungu
"Upendo wako mshikamanifu ni bora kuliko uhai" (3)
"Nimeridhika na fungu bora" (5)
Kutafakari kumhusu Mungu wakati wa usiku (6)
'Ninashikamana na Mungu' (8)
- 64 Ulinzi dhidi ya mashambulizi yaliyofichika
"Mungu atawapiga mishale" (7)
- 65 Mungu anaitunza dunia
"Msikiaji wa sala" (2)
"Mwenye furaha ni yule unayemchagua" (4)
Wema mwingi wa Mungu (11)
- 66 Kazi za Mungu zinazostaajibisha
"Njoooni mwone kazi za Mungu" (5)
"Nititimiza nadhiri zangu kwako" (13)
Mungu husikia sala (18-20)
- 67 Miisho ya dunia itamwogopa Mungu
Njia ya Mungu itajulikana (2)
'Mataifa yote na yamsifu Mungu' (3, 5)
"Mungu atatubariki" (6, 7)
- 68 'Maadui wa Mungu na watawanyike'
"Baba wa mayatima" (5)
Mungu huwapa makao walio wapweke (6)
Wanawake wanatangaza habari njema (11)
Wanaume kuwa zawadi (18)
'Yehova hutubebea mzigo wetu kila siku' (19)
- 69 Sala ya kuokolewa
"Bidii kwa ajili ya nyumba yako imenila" (9)
- "Nijibu haraka" (17)
'Walinipa siki ninywe' (21)
- 70 Aomba asaidiwe haraka
"Tenda haraka kwa niaba yangu" (5)
- 71 Tegemeo la waliozeeka
Kumtumaini Mungu tangu wakati wa ujana (5)
"Ninapoishiwa na nguvu" (9)
'Mungu amenifundisha tangu nilipokuwa kijana' (17)
- 72 Utawala wa amani wa mfalme aliyewekwa na Mungu
"Mwadilifu atasitawi" (7)
Raia kutoka bahari mpaka bahari (8)
Kuokolewa kutoka katika ukutili (14)
Nafaka itakuwa nyingi duniani (16)
Jina la Mungu lasifiwa milele (19)
- 73 Mtu aliyemwogopa Mungu arudiwa na ufahamu wa kiroho
"Hatua zangu zilikuwa karibu kuteleza" (2)
"Nilitaabika mchana kutwa" (14)
"Mpaka nilipoingia mahali patakatifu pa Mungu" (17)
Waovu wako kwenye ardhi yenye utelezi (18)
Kumkaribia Mungu ni jambo jema (28)
- 74 Asali Mungu awakumbuke watu wake
Matendo ya Mungu ya wokovu yakumbukwa (12-17)
"Kumbuka dhihaka za adui" (18)
- 75 Mungu ahukumu kwa haki
Waovu watakunywa kikombe cha Yehova (8)
- 76 Mungu atawashinda maadui wa Sayuni
Mungu awaokoa wapole (9)
Maadui wenye kiburi watanyenyekezwa (12)
- 77 Sala ya wakati wa taabu
Kutafakari kazi za Mungu (11, 12)
'Ee Mungu, ni nani aliyekuwa kama wewe?' (13)
- 78 Utunzaji wa Mungu na ukosefu wa imani wa Waisraeli
Kisimulie kizazi kijacho (2-8)
"Hawakudhihirisha imani katika Mungu" (22)
"Nafaka ya mbinguni" (24)

- "Wakamhuzunisha Mtakatifu wa Israeli" (41)
Kutoka Misri mpaka Nchi ya Ahadi (43-55)
"Waliendelea kumjaribu Mungu" (56)
- 79 Sala iliyotolewa mataifa yalipowavamia watu wa Mungu
'Sisi ni kitu cha kushutumiwa' (4)
'Tusaidie kwa ajili ya jina lako' (9)
"Waliipize jirani zetu mara saba" (12)
- 80 Mchungaji wa Israeli atafutwa ili awarudishe
"Ee Mungu, turudishe" (3)
Israeli, mzabibu wa Mungu (8-15)
- 81 Wahimizwa watii
Msiabudu miungu ya kigeni (9)
'Laiti mngesikiliza' (13)
- 82 Mwito wa kutekeleza hukumu ya haki Mungu anahukumu miongoni mwa "miungu" (1)
"Mteteeni mtu wa hali ya chini" (3)
"Ninyi ni miungu" (6)
- 83 Sala ya mtu anayekabili maadui
"Ee Mungu, usinyamaze" (1)
Maadui ni kama mwiba unaopeperushwa (13)
Jina la Mungu ni Yehova (18)
- 84 Kutamani sana hema tukufu la Mungu la ibada
Mlawi atamani kuwa kama ndege (3)
"Siku moja katika nyua zako" (10)
"Mungu ni jua na ngao" (11)
- 85 Sala ya kuomba warudishwe Mungu atawaambia washikamanifu wake kuhusu amani (8)
Upendo mshikamanifu utakutana na uaminifu (10)
- 86 Hakuna mungu aliye kama Yehova Yehova yuko tayari kusamehe (5)
Mataifa yote yatamwabudu Yehova (9)
'Nifundishe kuhusu njia yako' (11)
"Unganisha moyo wangu" (11)
- 87 Sayuni, jiji la Mungu wa kweli Waliozaliwa Sayuni (4-6)
- 88 Sala ya kuomba ulinzi dhidi ya kifo
"Uhai wangu uko kwenye kingo za Kaburi" (3)
'Kila asubuhi ninasali kwako' (13)
- 89 Kuimba kuhusu upendo mshikamanifu wa Yehova
Agano pamoja na Daudi (3)
Uzao wa Daudi utadumu milele (4)
Mtiwa-mafuta wa Mungu amwita Yeye "Baba" (26)
Agano la Daudi ni hakika (34-37)
Mwanadamu hawezi kuponyoka Kaburi (48)
- 90 Mungu wa milele na mwanadamu anayeishi kwa muda mfupi
Miaka elfu moja ni kama jana (4)
Mwanadamu anaishi miaka 70-80 (10)
"Tufundishe jinsi ya kuhesabu siku zetu" (12)
- 91 Ulinzi mahali pa siri pa Mungu
Kuokolewa kutoka kwa mwindaji wa ndege (3)
Kukumbilia chini ya mabawa ya Mungu (4)
Usalama hata elfu moja wakianguka (7)
Malaiika waagizwa kutoa ulinzi (11)
- 92 Yehova akwezwa milele
Kazi zake kuu na mawazo yake yenye kina (5)
'Waadilifu watasitawi kama mti' (12)
Waliozeeka wataendelea kunawiri (14)
- 93 Utawala wa Yehova wenye utukufu
"Yehova amekuwa Mfalme!" (1)
"Vikumbusho vyako vinategemeka" (5)
- 94 Sala ya kuomba Mungu alipize kisasi
"Waovu wataendelea mpaka lini?" (3)
Kurekebishwa na Yah huleta furaha (12)
Mungu hatawaacha watu wake (14)
'Kutunga matatizo kwa kutumia sheria' (20)
- 95 Ibada ya kweli pamoja na utii
"Leo ikiwa mtaisikiliza sauti yake" (7)
"Msiufanye moyo wenu kuwa mgumu" (8)
"Hawataingia katika pumziko langu" (11)
- 96 "Mwimbieni Yehova wimbo mpya"
Yehova anastahili kusifiwa kuliko wote (4)

- Miungu ya mataifa ni ubatili (5)
Abuduni katika mapambo
matakatifu (9)
- 97 Yehova amekwezwa juu ya miungu
mingine
"Yehova amekuwa Mfalme!" (1)
Mpendeni Yehova, chukieni
maovu (10)
Nuru kwa ajili ya mwadilifu (11)
- 98 Yehova ni Mwokozi na Mwamuzi
mwadilifu
Wokovu wa Yehova watangazwa (2, 3)
- 99 Yehova ni Mfalme mtakatifu
Ameketi kwenye kiti cha ufalme juu
ya makerubi (1)
Mungu anayesamehe na kuadhibu (8)
- 100 Kumshukuru Muumba
"Mtumikieni Yehova kwa
kushangilia" (2)
'Ni Mungu aliyetuumba' (3)
- 101 Mtawala anayetenda kwa utimilifu
'Sitavumilia kiburi' (5)
"Nitawatazama waaminifu" (6)
- 102 Sala ya mtu aliyekandamizwa,
anapokuwa amekata tamaa
"Mimi ni kama ndege aliye peke
yake" (7)
'Siku zangu ni kivuli kinachofifia' (11)
"Yehova atalijenga upya Sayuni" (16)
Yehova hudumu milele (26, 27)
- 103 "Nafsi yangu na imsifu Yehova"
Mungu huweka dhambi zetu mbali
sana (12)
Mungu huonyesha rehema kama
baba (13)
Mungu hukumbuka kwamba sisi ni
mavumbi (14)
Kiti cha ufalme cha Yehova na ufalme
wake (19)
Malaika hutekeleza neno la
Mungu (20)
- 104 Kumsifu Mungu kwa sababu ya
maajabu ya uumbaji
Dunia itadumu milele (5)
Divai na mkate kwa ajili ya
mwanadamu anayeweza kufa (15)
"Jinsi kazi zako zilivyo nyingi
sana!" (24)
'Roho inapoondolewa, wanakufa' (29)
- 105 Matendo ya uaminifu ya Yehova
kuelekea watu wake
Mungu anakumbuka agano lake (8-10)
"Msiwaguse watiwa-mafuta
wangu" (15)
Yosefu aliye utumwani atumiwa na
Mungu (17-22)
Miujiza ya Mungu nchini Misri (23-36)
Waisraeli watoka Misri (37-39)
Mungu akumbuka agano alilofanya
pamoja na Abrahamu (42)
- 106 Waisraeli wakosa kuthamini
Walisahau haraka matendo ya
Mungu (13)
Walibadili utukufu wa Mungu kwa
mfano wa ng'ombe dume (19, 20)
Hawakuwa na imani katika ahadi ya
Mungu (24)
Walijiunga na ibada ya Baali (28)
Watoto watolewa dhabihu kwa roho
waovu (37)
- 107 Mshukuruni Mungu kwa sababu ya
kazi zake zinazostaajibisha
Aliwaongoza katika njia inayofaa (7)
Aliwatoshesha wenye kiu na wenye
njaa (9)
Aliwatoa gizani (14)
Alituma neno lake kuwaponya (20)
Huwalinda maskini ili
wasikandamizwe (41)
- 108 Sala ya ushindi dhidi ya maadui
Wokovu kutoka kwa wanadamu
hauna faida yoyote (12)
"Kwa msaada wa Mungu tutapata
nguvu" (13)
- 109 Sala ya mtu anayeteseka
"Mtu mwingine na achukue cheo
chake" (8)
Mungu husimama mkono wa kulia
wa maskini (31)
- 110 Mfalme na kuhani kama Melkizedeki
'Tawala kati ya maadui wako' (2)
Vijana wanaojitoa kwa hiari ni kama
matone ya umande (3)
- 111 Msifuni Yehova kwa sababu ya kazi
zake kuu
Jina la Mungu ni takatifu na
linaogopesha (9)
Kumwogopa Yehova ni hekima (10)
- 112 Mwadilifu humwogopa Yehova
Mtu anayekopesha kwa ukarimu
atafanikiwa (5)

- “Mwadilifu atakumbukwa milele” (6)
Mtu mkarimu huwapa maskini (9)
- 113 Mungu aliye juu humwinua mtu wa hali ya chini
Jina la Yehova lasifiwa milele (2)
Mungu huinama chini (6)
- 114 Waisraeli wakombolewa kutoka Misri Bahari ilikimbia (5)
Milima ilirukaruka kama kondoo dume (6)
Mwamba mgumu wabadilishwa kuwa chemchemi za maji (8)
- 115 Mungu peke yake ndiye anayepaswa kutukuzwa
Sanamu zisizo na uhai (4-8)
Wanadamu wamepewa dunia (16)
“Watu waliokufa hawamsifu Yah” (17)
- 116 Wimbo wa shukrani
“Nitamlipa Yehova nini?” (12)
“Nitakiinua kikombe cha wokovu” (13)
“Nitamtimizia Yehova nadhiri zangu” (14, 18)
Kifo cha washikamanifu kina thamani (15)
- 117 Mataifa yote yahimizwa yamsifu Yehova
Upendo mshikamanifu wa Mungu ni mkubwa (2)
- 118 Kushukuru kwa sababu ya ushindi wa Yehova
‘Nilimlilia Yah, naye akanijibu’ (5)
“Yehova yuko upande wangu” (6, 7)
Jiwe lililokataliwa litakuwa jiwe kuu la pembeni (22)
“Yule anayekuja katika jina la Yehova” (26)
- 119 Kulithamini neno la Mungu lenye thamani
‘Vijana wanaweza kuisafishaje njia yao?’ (9)
“Ninavipenda sana vikumbusho vyako” (24)
“Neno lako ni tumaini langu” (74, 81, 114)
“Jinsi ninavyoipenda sana sheria yako!” (97)
“Ufahamu mwingi kuliko walimu wangu wote” (99)
“Neno lako ni taa ya mguu wangu” (105)
- ‘Kiini cha neno lako ni kweli’ (160)
Wanaoipenda sheria ya Mungu wana amani (165)
- 120 Mgeni atamani amani
‘Niokoe kutoka kwa ulimi mdanganyifu’ (2)
“Mimi ni mtu wa amani” (7)
- 121 Yehova huwalinda watu wake
“Msaada wangu hutoka kwa Yehova” (2)
Yehova halali usingizi kamwe (3, 4)
- 122 Sala ya kuomba jiji la Yerusalemu liwe na amani
Shangwe ya kwenda katika nyumba ya Yehova (1)
Jiji lililounganishwa pamoja kama kitu kimoja (3)
- 123 Kumtazama Yehova ili kupata kibali
‘Kama watumishi, tunamtazama Yehova’ (2)
“Tumedharauliwa vya kutosha” (3)
- 124 “Kama Yehova hangekuwa pamoja nasi”
Ponyoka kutoka katika mtego uliovonjika (7)
‘Jina la Yehova ni msaaada wetu’ (8)
- 125 Yehova huwalinda watu wake
“Kama milima inavyozunguka Yerusalemu” (2)
“Amani na iwe juu ya Israeli” (5)
- 126 Sayuni litarudishwa kwa shangwe
‘Yehova ametenda mambo makuu’ (3)
Baada ya kutokwa na machozi, kutakuwa na shangwe (5, 6)
- 127 Bila Mungu, kila kitu ni bure
“Yehova asipoienga nyumba” (1)
Watoto ni thawabu kutoka kwa Mungu (3)
- 128 Furaha kwa sababu ya kumwogopa Yehova
Mke kama mzabibu unaozaa matunda mengi (3)
“Na uone Yerusalemu likipata ufanisi” (5)
- 129 Ashambuliwa lakini hakushindwa
Wanaolichukia Sayuni waaibishwa (5)
- 130 “Kutoka vilindini ninakulilia”
‘Ikiwa ungekuwa unatazama makosa’ (3)

- Msamaha wa kweli hutoka kwa
Yehova (4)
"Ninamngojea Yehova kwa hamu" (6)
- 131 Kuridhika kama mtoto aliyeachishwa
kunyonya
Kutotafuta mambo makubwa sana (1)
- 132 Daudi achaguliwa na pia Sayuni
"Usimkatae mtiwa-mafuta wako" (10)
Makuhani wa Sayuni wavishwa
wokovu (16)
- 133 Kuka pamoja kwa umoja
Kama mafuta kwenye kichwa cha
Haruni (2)
Kama umande wa Hermoni (3)
- 134 Kumsifu Mungu nyakati za usiku
"Inueni mikono yenu katika
utakatifu" (2)
- 135 Msifuni Yah kwa sababu ya ukuu wake
Ishara na miujiza dhidi ya Misri (8, 9)
"Jina lako linadumu milele" (13)
Sanamu zisizo na uhai (15-18)
- 136 Upendo mshikamanifu wa Yehova
hudumu milele
Mbingu na dunia ziliumbwa kwa
ustadi (5, 6)
Farao alikufa katika Bahari
Nyekundu (15)
Mungu huwakumbuka walioshuka
moyo (23)
Huwapa chakula viumbe wote walio
hai (25)
- 137 Kando ya mito ya Babiloni
Nyimbo za Sayuni hazikuimbwa (3, 4)
Babiloni kuangamizwa (8)
- 138 Mungu anajali, ingawa amekwezwa
'Ulijibu sala yangu' (3)
'Hata katikati ya hatari,
unaniokoa' (7)
- 139 Mungu anawajua vizuri watumishi
wake
Huwezi kujificha mbali na roho ya
Mungu (7)
'Nimeumbwa kwa njia
inayostaajibisha' (14)
'Uliniona nikiwa kiinitete' (16)
"Uniongoze katika njia ya milele" (24)
- 140 Yehova ni Mwokozi mwenye nguvu
Waovu ni kama nyoka (3)
Watu wakatili wataangamia (11)
- 141 Sala ya kuomba ulinzi
- 'Sala yangu na iwe kama uvumba' (2)
Karipio la mwadilifu ni kama
mafuta (5)
Waovu wanaanguka ndani ya nyavu
zao wenyewe (10)
- 142 Sala ya kuomba aokolewe kutoka kwa
watesaji
"Sina mahali popote pa
kukimbilia" (4)
"Ni wewe tu niliye nawe" (5)
- 143 Kiu kwa ajili ya Mungu kama nchi
iliyokauka
'Ninatafakari kazi zako' (5)
"Nifundishe kufanya mapenzi
yako" (10)
'Roho yako nzuri na iniongoze' (10)
- 144 Sala ya kuomba ushindi
'Mwanadamu anayeweza kufa ni
nini?' (3)
'Maadui na watawanywe' (6)
Watu wa Yehova ni wenye furaha (15)
- 145 Kumsifu Mungu, Mfalme mkuu
'Nitatangaza ukuu wa Mungu' (6)
"Yehova ni mwema kwa wote" (9)
"Washikamanifu wako
watakusifu" (10)
Ufalme wa Mungu ni wa milele (13)
Mkono wa Mungu huwatosheleza
wote (16)
- 146 Mtumaini Mungu, si wanadamu
Mawazo ya mwanadamu hupotea
anapokufa (4)
Mungu huwainua juu walioinama
chini (8)
- 147 Kuzisifu kazi za Mungu za upendo na
zenye nguvu
Huwaponya waliovunjika moyo (3)
Huziita nyota zote kwa majina (4)
Hutoa theluji kama sufu (16)
- 148 Umbaji wote na umsifu Yehova
"Msifuni, enyi malaika wake wote" (2)
'Msifuni, jua, mwezi, na nyota' (3)
Vijana kwa wazee na wamsifu
Mungu (12, 13)
- 149 Wimbo wa kuusifu ushindi wa Mungu
Mungu anawafurahia watu wake (4)
Heshima ni ya washikamanifu wa
Mungu (9)
- 150 Kila kitu kinachopumua na kimsifu Yah
Haleluya! (1, 6)

KITABU CHA KWANZA
(Zaburi 1-41)

- 1** Mwenye furaha ni mtu ambaye hatembe katika mashauri ya waovu Na hasimami katika njia ya watenda dhambi^a Naye haketi katika kiti cha wenye dhihaka.^b
- 2** Lakini anapendezwa na sheria ya Yehova,^c Naye huisoma sheria Yake kwa sauti ya chini* mchana na usiku.^d
- 3** Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, Mti unaozaa matunda katika majira yake, Na majani yake hayanyauki. Na kila jambo analofanya litafanikiwa.^e
- 4** Waovu hawako hivyo; Wao ni kama makapi yanoyopeperushwa mbali na upepo.
- 5** Ndiyo sababu waovu hawataendelea kusimama katika hukumu;^f Wala watenda dhambi hawataendelea kusimama katika kusanyiko la waadilifu.^g
- 6** Kwa maana Yehova anaijua njia ya waadilifu,^h Lakini njia ya waovu itaangamia.ⁱ
- 2** Kwa nini mataifa yana msukosuko Na watu wananong'ona* kuhusu jambo lisilo na maana?^j
- 2** Wafalme wa dunia wanajipanga

SURA YA 1

a Met 4:14

b Met 22:10

c Zb 19:7
Zb 40:8
Zb 112:1
Mt 5:3
Ro 7:22
Yak 1:25d Yos 1:8
Zb 119:97
1Ti 4:15e 1Nya 22:13
Yer 17:7, 8

f Mt 25:41

g Mal 3:18
Mt 13:49, 50h Zb 37:18
Yer 12:3
1Pe 3:12

i Met 14:12

SURA YA 2

j Mdo 4:25-28

Safu ya 2

a Mt 27:1, 2
Lu 23:10, 11
Ufu 19:19b Zb 89:20
Isa 61:1c Zb 45:6
Eze 21:27
Da 7:13, 14
Ufu 19:16d 2Sa 5:7
Ufu 14:1e Mt 3:16, 17
Mk 1:9-11
Ro 1:4f Mdo 13:33
Ebr 1:5
Ebr 5:5g Zb 72:8
Ebr 1:2
Ufu 11:15h Ufu 12:5
Ufu 19:15i Da 2:44
Ufu 2:26, 27

Na maofisa wakuu wanakusanyika* pamoja kama kitu kimoja^a

Dhidi ya Yehova na dhidi ya mtiwa-mafuta[#] wake.^b

3 Wanasema: "Na tuzikate pingu zao

Na kuzitupa kamba zao!"

4 Yule anayeketi kwenye kiti cha ufalme mbinguni atacheka;

Yehova atawadhihaki.

5 Wakati huo ataongea nao kwa hasira yake

Na kuwatisha kwa hasira yake inayowaka,

6 Akisema: "Mimi mwenyewe nimemweka mfalme wangu^c

Juu ya Sayuni,^d mlima wangu mtakatifu."

7 Acheni nitangaze agizo la Yehova;

Aliniambia: "Wewe ni mwanangu;^e

Leo nimekuwa baba yako.^f

8 Niombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako

Na miisho ya dunia kuwa miliki yako.^g

9 Utawavunja kwa fimbo ya mfalme ya chuma,^h

Nawe utawavunjavunja kama chombo cha udongo."ⁱ

10 Basi sasa, enyi wafalme, onyesheni ufahamu;

Kubalini kurekebisha,^{*} enyi waamuzi wa dunia.

11 Mtumikieni Yehova kwa woga,

1:2 *Au "huitafakari sheria Yake." 2:1 *Au "wanatafakari kuhusu."

2:2 *Au "wanashauriana." #Au "Kri-sto." 2:10 *Au "onyo."

Na mshangilie mkitete-
meka.

- 12 Mheshimuni* mwana,^a la
siyyo Mungu atawaka ha-
sira

Nanyi mtaangamia kutoka
njiani,^b

Kwa maana hasira Yake
huwaka upesi.

Wenye furaha ni wale wote
wanaomkimbilia Yeye.

Muziki wa Daudi alipokuwa
akimkimbia Absalomu mwanawe.^c

- 3 Ee Yehova, kwa nini maa-
dui wangu wamekuwa
wengi sana?^d

Kwa nini watu wengi sana
wanainuka dhidi yangu?^e

- 2 Wengi wanasema hivi
kunihusu:*

“Mungu hatamwoko.”^f
(Sela)[#]

- 3 Lakini wewe, Ee Yehova,
ni ngao kunizunguka,^g
Utukufu wangu^h na Yule
anayekiinua kichwa cha-
ngu.ⁱ

- 4 Nitamlilia Yehova kwa
sauti kubwa,

Naye atanijibu kutoka
kwenye mlima wake
mtakatifu.^j (Sela)

- 5 Nitajilaza chini na kulala
usingizi;

Nami nitaamka nikiwa sa-
lama,

Kwa maana Yehova anaen-
delea kunitegemeza.^k

- 6 Siogopi makumi ya maelfu
Waliojipanga dhidi yangu
kila upande.^l

- 7 Inuka, Ee Yehova!
Niokoe,^m Ee Mungu
wangu!

Kwa maana utawapiga

SURA YA 2

a Flp 2:9-11

b Yoh 3:36

SURA YA 3

c 2Sa 15:14

d 2Sa 15:12
2Sa 16:15

e 2Sa 12:11

f 2Sa 16:7, 8

g Mwa 15:1

h Isa 45:25

i Zb 27:6

j 2Sa 15:25
Zb 2:6

k Zb 4:8
Met 3:24

l 2Fa 6:15, 16
Zb 27:3
Ro 8:31

m 1Ti 4:10

Safu ya 2

a 2Th 1:6

b Zb 37:39
Isa 43:11
Ufu 19:1

SURA YA 4

c Zb 11:7

d Efe 4:26

e Zb 37:3
Zb 62:8
Met 3:5
1Pe 4:19

f Hes 6:26
Zb 80:7
Met 16:15
1Pe 3:12

maadui wangu wote
kwenye utaya;

Utayavunja meno ya
waovu.^a

- 8 Wokovu ni wa Yehova.^b
Baraka yako iko juu ya
watu wako. (Sela)

Kwa kiongozi; uimbwe kwa
vinanda. Muziki wa Daudi.

- 4 Ninapokuita, unijibu,
Ee Mungu wangu
mwadilifu.^c

Nitengenezee njia ya kuto-
roka* taabu yangu.

Nionyeshe kibali na usikie
sala yangu.

- 2 Enyi wanadamu,
mtaendelea mpaka lini
kuibadili heshima yangu
kuwa aibu?

Mtaendelea mpaka lini
kupenda mambo yasiyo
na faida na kutafuta
mambo ya uwongo?
(Sela)

- 3 Jueni kwamba Yehova
atamtendea mshikama-
nifu wake kwa njia ya
pekee;*

Yehova atasikia ninapo-
mlilia.

- 4 Kasirika, lakini usitende
dhambi.^d

Zungumza moyoni mwako,
kitandani mwako, na
unyamaze kimya. (Sela)

- 5 Toa dhabihu za uadilifu,
Na umtumaini Yehova.^e

- 6 Kuna wengi wanaosema:
“Ni nani atakayetuonye-
sha jambo lolote jema?”
Acha nuru ya uso wako
ituangazie, Ee Yehova.^f

4:1 *Tnn., “Nitengenezee nafasi pana katika.” 4:3 *Au “atamfanya mshikamanifu wake aonekane kuwa tofauti; atamtenga kando mshikamanifu wake kwa ajili yake mwenyewe.”

2:12 *Tnn., “Mbusuni.” 3:2 *Au “kuihusu nafsi yangu.” #Angalia Kamusi, uku. 2012.

- 7 Umejaza moyo wangu shangwe nyingi sana
Kuliko wale walio na mavuno mengi sana ya nafaka na divai mpya.
- 8 Nitajilaza chini na kulala usingizi kwa amani,^a
Kwa maana wewe peke yako, Ee Yehova, hunifanya niishi kwa usalama.^b
- Kwa kiongozi wa Nehilothi.*
Muziki wa Daudi.
- 5 Sikiliza maneno yangu, Ee Yehova;^c
Sikiliza kwa makini kilio changu cha uchungu.
- 2 Sikiliza kilio changu cha kuomba msaada,
Ee Mfalme wangu na Mungu wangu, kwa sababu ninasali kwako.
- 3 Ee Yehova, utasikia sauti yangu asubuhi;^d
Asubuhi nitakueleza mahangaiko yangu^e na kusubiri kwa hamu.
- 4 Kwa maana wewe si Mungu anayefurahia uovu;^f
Hakuna mtu yeyote mwovu anayeweza kukaa nawe.^g
- 5 Hakuna mtu yeyote mwenye kiburi anayeweza kusimama mbele zako.*
Unawachukia wale wote wanaotenda maovu;^h
- 6 Utawaangamiza wale wanaosema uwongo.ⁱ
Yehova anawachukia kabisa watu wakati na wadanganyifu.*^j
- 7 Lakini nitaingia katika nyumba yako^k kwa saba-

5:Uta * Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:5 *Tnn., "katika uwepo wako." 5:6 *Au "anamchukia mtu anayemwaga damu na ambaye ni mdanganyifu."

SURA YA 4

a Zb 3:5
Met 3:24, 26

b Law 25:18

SURA YA 5

c Zb 65:2
1Pe 3:12

d Zb 55:16, 17

e Mk 1:35

f Zb 89:14
Met 6:16-19
Hab 1:13

g Zb 15:1-5
Met 12:19

h Ro 12:9
Ebr 1:9

i Met 20:19
Yoh 8:44
Kol 3:9
Ufu 21:8

j Mwa 9:6
Zb 55:23
Met 6:16, 17
1Pe 3:10

k 1Sa 3:3
1Nya 16:1

Safu ya 2

a Zb 69:13

b Zb 28:2
Zb 138:2

c Zb 25:4, 5
Zb 27:11

d Met 29:5
Ro 3:13

e 2Sa 15:31
2Sa 17:23
Zb 7:14, 15

f Zb 40:16

g Mwa 15:1
Zb 3:3

bu ya upendo wako mwingi mshikamanifu;^a
Nitainama chini kuelekea hekalu lako takatifu* nikiwa na heshima na woga kukuelekea.^b

- 8 Niongoze, Ee Yehova, katika uadilifu wako kwa sababu ya maadui wangu;
Ifanye njia yako iwe wazi kwangu.^c
- 9 Kwa maana hakuna lolote wanalosema linaloweza kutumainiwa;
Ndani yao hamna lolote isipokuwa nia ya kudhuru.
Koo lao ni kaburi lililo wazi;
Wanasifusifu kwa ulimi wao.*^d
- 10 Lakini Mungu atawatanga za kuwa na hatia;
Njama zao wenyewe zita-sababisha waanguke.^e
Na wafukuzwe kwa sababu ya dhambi zao nyingi, Kwa maana wamekuasi wewe.
- 11 Lakini wale wote wanaokukimbilia watashangilia;^f
Watapaza sauti kwa shangwe daima.
Nawe utawakinga wasifikiwe,
Na wale wanaolipenda jina lako watashangilia kwa sababu yako.
- 12 Kwa maana utambariki yeyote aliye mwadilifu, Ee Yehova;
Utawazunguka kwa kibali kana kwamba kwa ngao kubwa.^g

5:7 *Au "mahali pako patakatifu." 5:9 *Au "Wanatumia ulimi laini."

Kwa kiongozi; uimbwe kwa vinanda vilivyopatanishwa na sauti ya Sheminithi.* Muziki wa Daudi.

- 6** Ee Yehova, usinikaripie katika hasira yako, Na usinirekebishe katika ghadhabu yako.^a
- 2** Nionyeshe kibali,* Ee Yehova, kwa maana ninadhoofika. Niponye, Ee Yehova,^b kwa maana mifupa yangu inatetemeka.
- 3** Naam, ninasumbuka* sana,^c Nami nakuuliza, Ee Yehova—nitasumbuka mpaka lini?^d
- 4** Rudi, Ee Yehova, unio-koe;^{*e} Niokoe kwa ajili ya upendo wako mshikamanifu.^f
- 5** Kwa maana waliokufa hawakutaji;* Katika kaburi,[#] ni nani atakayekusifu?^g
- 6** Nimechoka kwa sababu ya kulia kwa uchungu;^h Usiku kucha ninakilowesha kitanda changu kwa machozi;* Kochi langu nalifanya lifurike kwa machozi.ⁱ
- 7** Jicho langu limedhoofika kwa sababu ya huzuni yangu;^j Limeingia giza* kwa sababu ya wote wanaoninyanyasa.
- 8** Niondokeeni, ninyi nyote mnaotenda maovu,

6:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. **6:2** *Au "rehema." **6:3** *Au "nafsi yangu inasumbuka." **6:4** *Au "uio-koe nafsi yangu." **6:5** *Au "hawakukumbuki." [#]Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. **6:6** *Tnn., "ninakifanya kitanda changu kiogelea." **6:7** *Au "Li-mezeeka."

SURA YA 6

a Zb 38:1
Yer 10:24

b Zb 41:4
Zb 103:2, 3

c Mt 26:38, 39

d Zb 13:1, 2

e Zb 50:15

f Zb 119:88
Omb 3:22

g Zb 30:9
Zb 115:17
Mhu 9:5, 10

h Zb 69:3

i Zb 39:12

j Zb 31:9

Safu ya 2

a Zb 3:4
Zb 145:18, 19
Ebr 5:7

b Zb 31:22
Zb 40:1
Yon 2:2

c Zb 40:14
Yer 20:11

SURA YA 7

d Zb 18:2
Met 18:10

e Yer 15:15
Zko 4:9
2Pe 2:9

f Zb 10:9

g Met 17:13

Kwa maana Yehova atasikia sauti ya kilio changu.^a

- 9** Yehova atasikia ombi langu la kutaka kibali;^b Yehova ataikubali sala yangu.
- 10** Maadui wangu wote wataaibishwa na kutamaushwa; Watarudi nyuma ghafla kwa aibu.^c
- Wimbo wa huzuni* wa Daudi ambao alimwambia Yehova kwa sababu ya maneno ya Kushi Mbenjamini.
- 7** Ee Yehova Mungu wangu, nimekukimbilia wewe.^d Niokoe kutoka kwa wale wote wanaonitesa na unifanye nisalimike.^e
- 2** La sivyo watanirua* vipandevipande kama simba anavyofanya,^f Watanibeba na kwenda nami pasipo na yeyote wa kuniokoa.
- 3** Ee Yehova Mungu wangu, ikiwa nimekosea katika jambo hili, Ikiwa nimetenda isivyo haki,
- 4** Ikiwa nimemkosea anayenitendea wema,^g Au ikiwa nimempora adui yangu bila sababu,*
- 5** Basi acha adui anikimbize na kunipita;* Acha aukanyagie uhai wangu ardhini Na kuufanya utukufu wangu utokomee mavu-mbini. (*Sela*)

7:Uta *Au "Wimbo wa maombolezo. **7:2** *Au "watairua nafsi yangu." **7:4** *Au labda, "Nilipomwacha hai yule anayenipinga bila sababu." **7:5** *Au "na kuipita nafsi yangu."

- 6** Inuka katika hasira yako,
Ee Yehova;
Simama ukabiliane na
hasira kali ya maadui wa-
ngu;^a
Amka kwa ajili yangu,
na uamuru kwamba haki
itendeke.^b
- 7** Acha mataifa yakuzingire;
Nawe utachukua hatua
dhidi yao kutoka juu.
- 8** Yehova atayahukumu
mataifa.^c
Nihukumu, Ee Yehova,
kulingana na uadilifu
wangu
Na kulingana na utimilifu
wangu.^d
- 9** Tafadhali, yakomeshe ma-
tendo maovu ya waovu.
Lakini umwimarisha
mwadilifu,^e
Kwa kuwa wewe ni Mungu
mwadilifu^f anayechu-
nguza mioyo^g na hisia
zilizo ndani kabisa.^{*h}
- 10** Mungu ni ngao yangu,ⁱ
Mwokozi wa wale walio
wanyoofu moyoni.^j
- 11** Mungu ni Mwamuzi
mwadilifu,^k
Na Mungu huzitangaza
hukumu zake* kila siku.
- 12** Mtu yeyote asipotubu,^l
Yeye huunoa upanga
wake,^m
Huukunja upinde wake na
kuuweka tayari.ⁿ
- 13** Hutayarisha silaha zake
zinazoua;
Huweka tayari mishale
yake inayowaka moto.^o
- 14** Mtazame yule aliye na
mimba ya uovu;
Hutunga mimba ya matati-
zo na kuzaa uwongo.^p

7:9 *Au "anayekaribu mioyo na figo."
7:11 *Au "huvurumisha shutuma zake."

SURA YA 7

- a Zb 3:7
Zb 35:1
b Zb 103:6
c Mwa 18:25
Zb 9:7, 8
d Zb 18:20
Zb 26:11
Zb 41:12
e Zb 37:25
f Kum 32:4
Ufu 15:3
g 1Sa 16:7
h 1Nya 28:9
Yer 17:10
Ufu 2:23
i Mwa 15:1
Met 30:5
j Met 2:21
k Mwa 18:25
Zb 9:4
Zb 98:9
l Isa 55:7
m Kum 32:41
n Kum 32:21, 23
o Kum 32:42
p Yak 1:15

Safu ya 2

- a Est 7:10
Zb 10:2
Zb 35:7, 8
Zb 57:6
Met 26:27
b Est 9:24, 25
c Zb 35:28
d Isa 25:1
Ebr 13:15
Ufu 15:4
e Da 4:17

SURA YA 8

- f 1Fa 8:27
Zb 104:1
Zb 148:13
g Mt 21:16
Lu 10:21
1Ko 1:27
h Zb 19:1
Zb 104:19
Isa 40:26
Ro 1:20
i Mwa 1:29
Mwa 9:3
Zb 144:3
Mt 6:25, 30
Yoh 3:16
Mdo 14:17
Ebr 2:6-8

- 15** Huchimba shimo na
kuzidisha kina chake,
Lakini huanguka katika
shimo hilohilo alilolichi-
mba.^a
- 16** Matatizo anayosababisha
yatarudi juu ya kichwa
chake mwenyewe;^b
Ukatili wake utaanguka
juu ya utosi wa kichwa
chake.
- 17** Nitamsifu Yehova kwa
sababu ya haki yake;^c
Nitaliambia sifa* jina la
Yehova^d Aliye Juu Zaidi.^e
Kwa kiongozi; juu ya Gitithi.*
Muziki wa Daudi.
- 8** Ee Yehova Bwana wetu,
jinsi jina lako lilivyo kuu
katika dunia yote;
Umeweka fahari yako
juu zaidi hata kuliko
mbingu!^{*f}
- 2** Kutoka katika vinywa
vya watoto wadogo na
wanaonyonya^g umeima-
risha nguvu
Kwa sababu ya maadui
wako,
Ili kumnyamazisha adui na
yule anayelipiza kisasi.
- 3** Ninapoziona mbingu zako,
kazi za vidole vyako,
Mwezi na nyota ambazo
umetayarisha,^h
- 4** Mwanadamu anayeweza
kufa ni nini hivi kwamba
unamweka akilini,
Na mwana wa mtu hivi
kwamba unamtunza?ⁱ
- 5** Ulimfanya awe mdogo
kidogo kuliko wale walio
kama Mungu,^{*}

7:17 *Au "Nitalipigia muziki." 8:Uta
*Angalia Kamusi, uku. 2012. 8:1 *Au
labda, "Wewe ambaye fahari yako inasi-
muliwa juu ya mbingu!" 8:5 *Au "kuli-
ko malaika."

Nawe ukamvika taji la utukufu na fahari.

- 6 Ulimpa mamlaka juu ya kazi za mikono yako;^a
Umeweka kila kitu chini ya miguu yake:
- 7 Kondoo wote na ng'ombe wote,
Na pia wanyama wa mwi-tuni,^b
- 8 Ndege wa angani na sama-ki wa baharini,
Kitu chochote kinachopita katika njia za baharini.
- 9 Ee Yehova Bwana wetu, jinsi jina lako lilivyo kuu katika dunia yote!

Kwa kiongozi; juu ya Muth-labeni.*
Muziki wa Daudi.

✠ [Aleph]

- 9 Nitakusifu, Ee Yehova, kwa moyo wangu wote; Nitasimulia kuhusu kazi zako zote zinazostaaja-bisha.^c
- 2 Nitafurahi na kushangilia kwa sababu yako; Nitaliambia sifa* jina lako, Ee Uliye Juu Zaidi.^d
- ✠ [Beth]
- 3 Maadui wangu wanapokimbia,^e
Watajikwaa na kuangamia kutoka mbele zako.
- 4 Kwa maana unatetea njia yangu ya haki;
Unaketi kwenye kiti chako cha ufalme ukihukumu kwa uadilifu.^f

✠ [Gimel]

- 5 Umeyakemea mataifa^g na kuwaangamiza waovu, Na hivyo kulifuta jina lao milele na milele.
- 6 Maadui wameangamizwa milele;

SURA YA 8

a Mwa 1:26
Mwa 9:1, 2

b Mwa 1:28
Mwa 9:3

SURA YA 9

c 1Nya 16:12
1Nya 29:11
Ufu 4:11

d Zb 28:7

e Zb 56:9

f Zb 89:14
1Pe 2:23

g Kum 9:4

Safu ya 2

a Kum 25:19

b Zb 90:2
1Ti 1:17

c Ro 14:10
Ufu 20:11

d Mwa 18:25
Zb 85:11
Isa 26:9

e Zb 96:13
Zb 98:9
Mdo 17:31

f Zb 91:2

g Zb 46:1
Zb 54:7

h Zb 91:14
Met 18:10
Yer 16:21

i 2Nya 20:12
Zb 25:15
2Ko 1:10

j Zb 96:10
Zb 107:19, 22
Isa 12:3, 4

k Mwa 4:9, 10
Mwa 9:5
Kum 32:43
2Fa 9:24, 26
2Fa 24:3, 4
Lu 11:49-51

l Kut 3:7
Zb 72:13, 14
Lu 18:7

m Zb 30:3
Isa 38:9, 10
Ufu 1:17, 18

Uliyang'oa majiji yao,
Na kumbukumbu lote
kuwahusu litatoweka.^a

✠ [He]

- 7 Lakini Yehova ameketi kwenye kiti cha ufalme milele;^b
Ameiimarisha kabisa kiti chake cha ufalme kwa ajili ya haki.^c
- 8 Ataihukumu kwa uadilifu dunia inayokaliwa;^d
Atayahukumu mataifa kwa kutoa maamuzi ya uadilifu.^e

✠ [Waw]

- 9 Yehova atakuwa kimbilio salama* kwa wanaokandamizwa,^f
Kimbilio salama katika nyakati za taabu.^g
- 10 Wale wanaolijua jina lako watakutumaini wewe;^h
Hutawaacha kamwe wale wanaokutafuta, Ee Yehova.ⁱ
- ✠ [Zayin]
- 11 Mwimbieni sifa Yehova, anayekaa Sayuni;
Tangazeni matendo yake miongoni mwa mataifa.^j
- 12 Kwa maana Yule anayelipi-za kisasi kwa ajili ya damu yao anawakumbuka;^k
Hatasahau kilio cha wanaoteseka.^l

✠ [Heth]

- 13 Nionyeshe kibali, Ee Yehova; angalia nina-vyoteswa na wale wanaonichukia,
Wewe unayeniinua kutoka katika malango ya kifo,^m
- 14 Ili nitangaze katika malango ya binti ya

9:Uta * Angalia Kamusi, uku. 2012. 9:2
*Au "Nitalipigia muziki."

9:9 *Au "kilele salama."

Sayuni matendo yako
yanayostahili sifa,^a

Na kushangilia kwa saba-
bu ya matendo yako ya
wokovu.^b

↳ [Teth]

15 Mataifa yamezama chini
katika shimo walilo-
chimba;

Mguu wao wenyewe ume-
naswa katika wavu
waliouficha.^c

16 Yehova anajulikana kwa
hukumu anazotekeleza.^d
Mwovu amenaswa katika
kazi za mikono yake
mwenyewe.^e

Higayoni.* (Sela)

* [Yod]

17 Waovu watageuka na
kuelekea Kaburini,*
Mataifa yote yanayomsa-
hau Mungu.

18 Lakini maskini hawatasa-
hauliwa daima;^f
Wala tumaini la wapole
halitapotea kamwe.^g

↳ [Kaph]

19 Inuka, Ee Yehova! Usiache
mwanadamu anayeweza
kufa ashinde.

Mataifa na yahukumiwe
mbele zako.*^h

20 Wapige kwa woga, Ee
Yehova,ⁱ

Acha mataifa yajue kwa-
mba wao ni wanadamu
tu wanaoweza kufa.
(Sela)

↳ [Lamed]

10 Ee Yehova, kwa nini
unasimama mbali?
Kwa nini unajificha
nyakati za taabu?^j

9:16 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
9:17 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi,
uku. 2012. **9:19** *Tnn., "mbele za uwe-
po wako."

SURA YA 9

a Yer 17:19, 20

b Zb 13:5
Zb 20:5

c Kum 32:35
Met 5:22

d Kut 14:4
Yos 2:10
2Fa 19:19

e Met 26:27
Isa 3:11

f Zb 12:5
Zb 72:4

g Zb 10:17
Mt 5:5

h Mwa 18:25
Zb 82:8

i Kut 15:16
Kut 23:27

SURA YA 10

j Zb 13:1
Zb 22:1
Yer 14:8

Safu ya 2

a Kut 14:17

b Zb 7:14, 16
Zb 37:7
Met 5:22
Met 26:27

c Kut 15:9
Ho 12:8

d Zb 14:1, 2
Zb 53:1
Sef 1:12

e Zb 37:35

f Isa 26:11
Ho 14:9

g Met 14:16
Mhu 8:11

h Ro 3:14

i Zb 7:14
Zb 12:2
Zb 55:21

j Met 1:10, 11

k Zb 17:9, 11

l Ayu 38:39, 40
Zb 17:12
Zb 59:3

2 Mwovu humfuatia kwa
kiburi mtu asiye na
uwezo,^a

Lakini atanaswa katika
njama anazopanga.^b

3 Kwa maana mwovu hujiga-
mba kuhusu tamaa zake
za kichoyo*^c
Naye humbariki mwenye
pupa;[#]

↳ [Nun]

Humkosea heshima
Yehova.

4 Kwa sababu ya kiburi
chake, mwovu hafanyi
uchunguzi wowote;
Mawazo yake yote ni:
"Hakuna Mungu."^d

5 Njia zake huendelea kufa-
nikiwa,^e

Lakini hukumu zako zime-
pita uelewaji wake;^f
Huwadhihaki* maadui
wake wote.

6 Anasema moyoni mwake:
"Sitatikiswa kamwe;*
Kizazi baada ya kizazi
Sitaona msiba kamwe."^g

↳ [Pe]

7 Kinywa chake kimejaa laa-
na, uwongo, na vitisho;^h
Chini ya ulimi wake kuna
taabu na madhara.ⁱ

8 Huvizia karibu na makao;
Kutoka mahali anapojifi-
cha humuua mtu asiye
na hatia.^j

↳ [Ayin]

Macho yake yanamtafuta
mtu asiye na kosa.^k

9 Hungojea mahali alipojifi-
cha kama simba katika
pango* lake.^l

10:3 *Au "tamaa ya nafsi yake." #Au
labda, "Mwenye pupa hujibariki mwe-
nyewe." **10:5** *Au "Hujitutumua kwa."
10:6 *Au "Sitapepesuka (Sitayumbu-
mba) kamwe." **10:9** *Au "pori."

Hungojea ili amkamate
asiye na uwezo.

Humkamata asiye na
uwezo anapouvuta
wavu wake na
kuufunga.^a

10 Mtu huyo hupondwa na
kuangushwa chini;

Watu wasio na kosa
huanguka mikononi
mwake.*

11 Yeye husema moyoni
mwake: “Mungu
amesahau.^b

Ameugeuzia mbali uso
wake.

Haoni kamwe.”^c

☞ [Qoph]

12 Inuka, Ee Yehova.^d Ee Mu-
ngu, inua mkono wako.^e
Usiwasahau wasio na
uwezo.^f

13 Kwa nini mwovu amemko-
sea Mungu heshima?
Husema moyoni mwake:
“Hutanifanya niwaji-
bike.”

☞ [Resh]

14 Lakini unaona mateso na
taabu.

Wewe huendelea kutazama
na kuchukua hatua.^g

Mtu huyo asiye na kosa
hukugeukia wewe;^h
Wewe ndiye msaidizi wa
yatima.ⁱ

☞ [Shin]

15 Uvunje mkono wa mtu
mwovu na mbaya,^j

Ili utakapoutafuta uovu
wake,

Hutaupata tena.

16 Yehova ni Mfalme milele
na milele.^k

Mataifa yameangamia
kutoka duniani.^l

10:10 *Au “katika makucha yake.”

SURA YA 10

a Zb 140:5
Yer 5:26

b Mhu 8:11

c Zb 73:3, 11
Zb 94:3, 7
Eze 8:12
Eze 9:9

d Zb 3:7

e Mik 5:9

f Zb 9:12
Zb 35:10

g 2Fa 9:26
2Nya 6:23

h 1Pe 4:19

i Kum 10:17, 18
Zb 146:9
Ebr 13:6

j Ayu 38:15

k Kut 15:18
Zb 145:13
Yer 10:10
Da 4:34
1Ti 1:17

l Zb 9:5
Zb 44:2

Safu ya 2

a Zb 9:18

b 1Nya 29:18, 19

c Met 15:8
1Pe 3:12

d Zb 72:4

e Isa 51:12

SURA YA 11

f 2Nya 14:11
Zb 7:1
Zb 56:11

g Mik 1:2
Hab 2:20

h 2Nya 20:6
Zb 103:19
Ufu 4:2, 3

i 2Nya 16:9
Met 15:3
Zek 4:10
Ebr 4:13

j Mwa 6:5
Mwa 7:1

k Met 3:31
Met 6:16, 17

☞ [Taw]

17 Lakini utasikia ombi la
wapole, Ee Yehova.^a

Utaiimarisha mioyo yao^b
na kuwasakiliza kwa
makini.^c

18 Utawatendea haki
mayatima na wale
wanaopondwa,^d

Ili mwanadamu anayeweza
kufa ambaye ni mavumbi
asiwaogopeshe tena.^e

Kwa kiongozi. Wa Daudi.

11 Nimemkimbilia Yehova.^f
Basi mnawezaje kunia-
mbia:*

“Kimbilia kwenye mlima
wako kama ndege!

2 Tazama jinsi waovu wana-
vyoukunja upinde;
Huutia mshale wao kwe-
nye kamba ya upinde,
Ili wawapige kutoka gizani
wale walio wanyoofu mo-
yoni.

3 Misingi* inapobomolewa,
Mtu mwadilifu anaweza
kufanya nini?”

4 Yehova yumo katika
hekalu lake takatifu.^g
Kiti cha ufalme cha Yeho-
va kiko mbinguni.^h

Macho yake mwenyewe
yanatazama, macho yake
yalioo makini* yanawa-
chunguza wanadamu.ⁱ

5 Yehova humchunguza
mwadilifu na pia
mwovu;^j

Humchukia* mtu yeyote
anayependa ukatili.^k

6 Atawanyeshea waovu
mitego;*

11:1 *Au “kuiambia nafsi yangu.” 11:3
*Au “Misingi ya haki.” 11:4 *Au “ya-
nayong’aa.” 11:5 *Au “Nafsi yake ina-
mchukia; Yeye binafsi anamchukia.”
11:6 *Au labda, “makaa ya mawe yana-
yowaka.”

Moto na kiberiti^a na upepo unaounguzwa vitakuwa fungu la kikombe chao.

- 7 Kwa maana Yehova ni mwadilifu;^b yeye hupe-
nda matendo ya
uadilifu.^c

Wanyoofu watauona uso wake.^{*d}

Kwa kiongozi; umepatanishwa na sauti ya Sheminithi.*
Muziki wa Daudi.

- 12** Niokoe, Ee Yehova, kwa maana mtu mshika-manifu hayupo tena;

Watu waaminifu wameto-weka kutoka miongoni mwa wanadamu.

- 2 Wanaambiana uwongo; Wanasifusifu kwa midomo yao* na kuzungumza kwa moyo midangan-nyifu.^{#e}

- 3 Yehova ataikata kabisa midomo yote inayosifu-sifu

Na ulimi unaojigamba kupindukia,^f

- 4 Wale wanaosema: "Tuta-shinda kwa ndimi zetu. Tunatumia midomo yetu tependavyo;

Ni nani atakayekuwa bwana mkubwa wetu?"^g

- 5 "Kwa sababu wale wanao-teswa wanakandamizwa, Kwa sababu ya kilio cha uchungu cha maskini,^h Nitainuka na kutenda," asema Yehova.

"Nitawaokoa kutoka kwa wale wanaowatendea kwa dharau."^{**}

11:7 *Au "watajionea kibali chake."
12:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.
12:2 *Tnn., "Wanaongea kwa mdomo laini." #Tnn., "kwa moyo na moyo."
12:5 *Au "wanaojitutumua mbele yao."

SURA YA 11

a Mwa 19:24
Eze 38:22

b Kum 32:4

c Zb 146:8

d Ayu 36:7
Zb 34:15
1Pe 3:12

SURA YA 12

e Zb 28:3

f Kut 15:9, 10
1Sa 2:3
Eze 28:2

g Zb 10:5

h Kut 3:7

Safu ya 2

a 2Sa 22:31
Zb 19:8

b 1Sa 2:9

c Mhu 8:11

SURA YA 13

d Ayu 13:24
Zb 6:3
Zb 22:2

e Zb 22:7, 8

f Zb 25:2
Zb 35:19

g Zb 52:8
Zb 147:11
1Pe 5:6, 7

h 1Sa 2:1

i Zb 116:7
Zb 119:17

- 6 Maneno ya Yehova ni safi;^a Ni kama fedha iliyosafi-shwa katika tanuru la udongo,* iliyosafishwa mara saba.

- 7 Utawalinda, Ee Yehova;^b Utamlinda kila mmoja wao milele kutokana na kiza-zi hiki.

- 8 Waovu wanatembea huku na huku kwa uhuru Kwa sababu wanadamu wanaendeleza upotovu.^c

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

- 13** Ee Yehova, utanisahau mpaka lini? Milele?

Utanificha uso wako mpaka lini?^d

- 2 Nitahangaika kwa wasiwa-si mpaka lini, Nikiwa na huzuni moyoni mwangu kila siku?

Adui yangu atanishinda mpaka lini?^e

- 3 Nitazame na unijibu, Ee Yehova Mungu wangu. Yatie nuru macho yangu, ili nisilale usingizi katika kifo,

- 4 Ili adui yangu asiseme: "Nimemshinda!"

Usiruhusu wapinzani wangu washangilie kuanguka kwangu.^f

- 5 Lakini mimi, ninautu-maini upendo wako mshikamanifu;^g

Moyo wangu utashangilia kwa sababu ya matendo yako ya wokovu.^h

- 6 Nitamwambia Yehova, kwa maana amenithawabisha kwelikweli.^{*i}

12:6 *Au labda, "tanuru la kuyeyusha lililowekwa ardhini." 13:6 *Au "ameshughulika nami kwa njia inayothawabisha."

Kwa kiongozi. Wa Daudi.

14 Mpumbavu* husema moyoni mwake:

“Hakuna Yehova.”^a

Matendo yao yamepotoka, na shughuli zao zinachukiza;

Hakuna yeyote anayete-nda mema.^b

2 Lakini Yehova anawatazama wanadamu kutoka mbinguni

Ili aone ikiwa kuna yeyote aliye na ufahamu, ikiwa kuna yeyote anayemtafuta Yehova.^c

3 Wote wamegeuka kando;^d Wote wamepotoka.

Hakuna yeyote anayete-nda mema, Hakuna hata mmoja.

4 Je, hakuna mtenda maovu yeyote anayelewa?

Wanawala watu wangu kana kwamba wanakula mkate.

Hawamwiti Yehova.

5 Lakini watajawa na hofu kubwa,^e

Kwa maana Yehova yuko pamoja na kizazi cha waadilifu.

6 Ninyi waovu hujaribu kuharibu mipango ya mtu wa hali ya chini, Lakini Yehova ni kimbilio lake.^f

7 Laiti wokovu wa Israeli ungetoka Sayuni!^g

Yehova anapowakusanya tena watu wake walio-tekwa,

Yakobo na ashangilie, Israeli na afurahi.

14:1 *Au “Asiyetumia akili.”

SURA YA 14

a Zb 10:4
Isa 29:16

b Zb 53
Ro 3:10-12

c 2Nya 16:9
Zb 33:13-15
Ebr 11:6

d Mhu 7:29

e Kut 15:16

f Zb 9:9
Zb 142:5

g Ro 11:26, 27

Safu ya 2

SURA YA 15

a Zb 2:6
Zb 24:3, 4

b Zb 1:1

c Isa 33:15, 16
Mdo 10:34, 35

d Met 3:32
Efe 4:25

e Law 19:16
Zb 101:5
Met 20:19

f Met 14:21
Ro 12:17

g Kut 23:1

h Est 3:2

i Yos 9:18-20
Amu 11:34, 35
Zb 50:14
Mt 5:33

j Kut 22:25

k Kut 23:8

l Zb 16:7, 8
Met 12:3
2Pe 1:10

SURA YA 16

m Zb 25:20

Muziki wa Daudi.

15 Ee Yehova, ni nani anayeweza kuwa mgeni katika hema lako?

Ni nani anayeweza kukaa katika mlima wako mta-katifu?^a

2 Yule anayetembea bila kosa,^{*b}

Anayezoea kutenda yaliyo sawa^c

Na kusema ukweli moyoni mwake.^d

3 Hachongeji kwa ulimi wake,^e

Hamtendei jirani yake jambo lolote ovu,^f

Naye hawaharibii sifa* rafiki zake.^g

4 Humkataa mtu yeyote anayedharauliwa,^h

Lakini huwaheshimu wale wanaomwogopa Yehova.

Havunji ahadi yake, hata ikimletea hasara.^{*i}

5 Hakopeshi pesa zake kwa faida,^j

Naye hakubali rushwa ili kumkandamiza asiye na hatia.^k

Yeyote anayefanya mambo hayo hatatikiswa kamwe.^{*l}

Miktamu* ya Daudi.

16 Nilinde, Ee Mungu, kwa maana nimekukimbilia wewe.^m

2 Nimemwambia Yehova: “Wewe ni Yehova, Chanzo changu cha wema.

3 Na watakatifu walio duni- niani,

15:2 *Au “kwa utimilifu.” 15:3 *Au “hawaabishi.” 15:4 *Tnn., “Havunji kipa- cho chake, hata kinapomletea hasara.” 15:5 *Au “hatapepesuka (hatayumba- yumba) kamwe.” 16:Uta *Angalia Ka- musi, uku. 2012.

Watukufu, ndio ninaope-
ndezwa nao sana.”^a

- 4 Wale wanaoifuatia miungu
mingine huzidisha huzu-
ni yao.^b

Sitamimina kamwe mato-
leo yao ya vinywaji ya
damu,

Wala midomo yangu haita-
taja majina yao.^c

- 5 Yehova ni fungu langu,
sehemu niliyogawiwa,^d
na kikombe changu.^e

Unaulinda urithi wangu.

- 6 Nimepimiwa sehemu
zinazopendeza.

Naam, nimeridhika na
urithi wangu.^f

- 7 Nitamsifu Yehova, ambaye
amenipa ushauri.^g

Hata wakati wa usiku,
mawazo yangu ya ndani
kabisa* hunirekebisha.^h

- 8 Ninamweka Yehova mbele
yangu daima.ⁱ

Kwa sababu yuko mkono
wangu wa kulia, sitatiki-
swa kamwe.^j

- 9 Kwa hiyo moyo wangu
unashangilia, nafsi yan-
gu yote ina* shangwe.
Nami ninaishi* kwa usa-
lama.

- 10 Kwa maana hutaniacha*
Kaburini.^k

Hutamruhusu mshikama-
nifu wako aone shimo.^l

- 11 Unanijulisha njia ya uzi-
ma.^m

Shangwe tele iko mbele
zako;ⁿ

16:7 *Au “hisia zangu za ndani kabi-
sa.” Tnn., “figo zangu.” 16:8 *Au “sita-
pepesuka (sitayumbayumba) kamwe.”
16:9 *Tnn., “utukufu wangu una.” *Au
“Mwili wangu huishi.” 16:10 *Au “hu-
taiacha nafsi yangu.” *Au “Sheoli.”
Angalia Kamusi, uku. 2012. ^aAu labda,
“aone uharibifu.” 16:11 *Tnn., “pamoja
na uso wako.”

SURA YA 16

a Zb 119:63

b Kum 8:19
Zb 97:7
Yon 2:8

c Kut 23:13
Yos 23:6, 7

d Zb 73:26

e Zb 23:5

f Zb 78:55

g Isa 48:17

h Zb 17:3
Zb 26:2

i Zb 139:17, 18

j Zb 73:23
Mdo 2:25-28

k Zb 49:15
Mdo 2:31
Mdo 3:15
Ufu 1:17, 18

l Ayu 14:13, 14
Mdo 13:34-37

m Met 12:28

n Zb 21:6
Mt 5:8

Safu ya 2

SURA YA 17

a Zb 145:18

b Zb 37:5, 6

c Zb 11:5
Zb 16:7
1Ko 4:4

d Zb 26:2
Mal 3:3
Ipe 1:6, 7

e Zb 119:9

f Zb 18:36
Zb 94:18
Zb 119:133
Zb 121:3

g Zb 55:16

h Isa 37:17

i Zb 31:21
Omb 3:22

j Kum 32:9, 10
Zek 2:8

Kuna furaha* kwenye
mkono wako wa kuume
milele.

Sala ya Daudi.

- 17 Sikia sihi yangu ya kuo-
mba haki, Ee Yehova;

Sikiliza kilio changu cha
kuomba msaada;

Sikiliza sala yangu ninayo-
sema bila udanganyifu.^a

- 2 Nawe ufanye uamuzi wa
haki kwa niaba yangu;^b

Macho yako na yaone
yaliyo sawa.

- 3 Umechunguza moyo
wangu, umenikagua
wakati wa usiku;^c

Umenisafisha;^d

Utagundua kwamba sija-
panga njama ya kutenda
uovu wowote,

Na kinywa changu hakija-
tenda dhambi.

- 4 Kuhusiana na shughuli za
wanadamu,

Kulingana na neno la
midomo yako, ninaepuka
njia za mnyang’anyi.^e

- 5 Acha hatua zangu zibaki
kwenye njia zako

Ili miguu yangu isijikwae.^f

- 6 Ninakuita wewe, kwa
sababu utanijibu,^g Ee
Mungu.

Nitegee sikio lako.* Sikia
maneno yangu.^h

- 7 Onyesha upendo wako
mshikamanifu kwa njia
yenye kustaaajabisha,ⁱ

Ee Mwokozi wa wale
wanaokimbilia mkono
wako wa kuume

Kutoka kwa wale wanao-
kuasi.

- 8 Nilinde kama mboni ya
jicho lako;^j

16:11 *Au “uzuri.” 17:6 *Au “Inama chi-
ni na unisikilize.”

Nifiche katika kivuli cha mabawa yako.^a

- 9** Nilinde kutokana na waovu wanaoni-shambulia,
Kutokana na maadui wangu* wanaoweza kufa ambao wanazingira.^b
- 10** Wamekufa ganzi;*
Kwa kinywa chao wanao-
ngea kwa kiburi;
- 11** Sasa wanatuzingira;^c
Wanatafuta nafasi ya kutuangusha.*
- 12** Yeye ni kama simba anayetamani kurarua windo lake vipandevipande,
Kama mwanasimba anayenyemelea mafichoni.
- 13** Inuka, Ee Yehova, ukabiliane naye^d na kumwangusha chini;
Niokoe* kutoka kwa mwovu kwa kutumia upanga wako;
- 14** Niokoe kwa mkono wako, Ee Yehova,
Kutoka kwa watu wa ulimwengu huu,* ambao fungu lao liko katika maisha haya,^e
Wale ambao unawajaza kwa vitu vizuri unavyo-
ndaa^f
Na ambao huwaachia urithi wana wao wengi.
- 15** Lakini mimi, nitauona uso wako kwa sababu ya uadilifu wangu;
Ninaridhika kuamka mbele zako.*^g

17:9 *Au "maadui wangu walio dhidi ya nafsi." 17:10 *Au "Wamefunikwa na mafuta yao wenyewe." 17:11 *Au "kututupa chini." 17:13 *Au "lokoe nafsi yangu." 17:14 *Au "mfumo huu wa mambo." 17:15 *Au "kuona sura yako."

SURA YA 17

a Ru 2:12
Zb 36:7
Zb 57:1

b 1Sa 24:11
Zb 35:4

c 1Sa 23:26

d Zb 7:6

e Zb 73:12

f Mt 5:45

g Zb 65:4

Safu ya 2

SURA YA 18

a 2Sa 22:1

b Zb 18:32
Isa 12:2

c Zb 3:3
Zb 37:39, 40
Zb 40:17

d Kum 32:4

e Mwa 15:1
2Sa 22:2-4

f Zb 50:15

g 1Sa 20:3
Zb 116:3

h 2Sa 20:1
2Sa 22:5, 6
Zb 22:16

i Mhu 9:12

j Zb 11:4

k 2Sa 22:7
Zb 10:17
Zb 34:15
1Pe 3:12

l Amu 5:4

Kwa kiongozi. Wa Daudi mtumishi wa Yehova, aliyemwambia Yehova maneno ya wimbo huu siku ambayo Yehova alimwokoia kutoka mikononi mwa maadui wake wote na kutoka mikononi mwa Sauli. Alisema:^a

18 Ninakupenda, Ee Yehova, nguvu zangu.^b

2 Yehova ni jabali langu na ngome yangu na Mwokozi wangu.^c

Mungu wangu ni mwamba wangu,^d ninayemki-
mbilia,

Ngao yangu na pembe*
yangu ya wokovu,[#]
kimbilio langu salama.^{△e}

3 Ninamlilia Yehova, anayestahili kusifiwa,
Nami nitaokolewa kutoka kwa maadui wangu.^f

4 Kamba za kifo zilinizu-
nguka;^g
Mafuriko ya ghafla ya watu wasiofaa kitu yaliniogopesha.^h

5 Kamba za Kaburi* zilini-
zunguka;
Mitego ya kifo ilinikabili.ⁱ

6 Katika taabu yangu nili-
mwita Yehova,
Niliendelea kumlilia
Mungu wangu
anisaidie.

Akiwa katika hekalu lake aliisikia sauti yangu,^j

Na kilio changu cha kumwomba msaada kili-
fika masikioni mwake.^k

7 Kisha dunia ikaanza kute-
temeka na kutikisika;^l
Misingi ya milima ikasu-
kasuka

18:2 *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "mwokozi wangu mwenye nguvu." △Au "kilele changu salama." 18:5 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

Nayo ikatikisika huku na huku kwa sababu alikuwa amekasirishwa.^a

- 8** Moshi ulipanda kutoka katika mianzi ya pua yake, Na moto unaoteketeza kabisa ukatoka kinywani mwake;^b

Makaa ya mawe yanayowaka moto mkali yakatoka kwake.

- 9** Alizifanya mbingu zijikunje alipokuwa akishuka,^c Na giza zito lilikuwa chini ya miguu yake.^d

- 10** Alipanda juu ya kerubi, akaja akiruka.^e Akashuka chini kwa ghafla juu ya mabawa ya kiumbe wa roho.^{*f}

- 11** Kisha akajifunika giza,^g Pande zote kama banda, Maji yenye giza na mawingu mazito.^h

- 12** Kutoka katika mwangaza ulio mbele zake Mvua ya mawe na makaa ya mawe yanayowaka moto yakapasua mawingu.

- 13** Kisha Yehova akaanza kunguruma mbinguni;ⁱ Aliye Juu Zaidi aliifanya sauti yake isikike^j Kwa mvua ya mawe na makaa ya mawe yanayowaka moto.

- 14** Alipiga mishale yake akawatawanya;^k Alivurumisha radi yake akawavuruga.^l

- 15** Sakafu za vijito zikaonekana;^{*m} Misingi ya nchi ikafunuliwa kwa kemeo lako, Ee Yehova,

18:10 *Au "upepo." **18:15** *Au "Mifereji ya maji ikaonekana."

SURA YA 18

a 2Sa 22:8-16
Zb 77:18

b Isa 30:27

c Zb 144:5
Isa 64:1

d 2Sa 22:10

e Zb 99:1

f Zb 104:3
Ebr 1:7

g Zb 97:2

h Ayu 36:29

i 1Sa 2:10
1Sa 7:10

j 2Sa 22:14
Zb 29:3

k Isa 30:30

l Ayu 36:32
Zb 144:6

m Zb 74:15
Zb 106:9
Zb 114:1, 3

Safu ya 2

a Kut 15:8
2Sa 22:16

b 2Sa 22:17-20
Zb 124:2-4

c Zb 3:7

d Zb 35:10

e 1Sa 19:11
1Sa 23:26

f Zb 149:4

g 1Sa 26:23
1Fa 8:32

h 1Sa 24:11
2Sa 22:21-25
Zb 24:3, 4

i Zb 84:11

j 2Sa 22:24
Met 14:16

k Isa 3:10
Ebr 11:6

l 2Sa 22:25
Met 5:21

m Zb 97:10

Kwa mlipuko wa pumzi kutoka katika mianzi ya pua yako.^a

- 16** Aliunyoosha mkono wake kutoka juu;

Alinishika na kunivuta kutoka katika maji yenye kina.^b

- 17** Aliniokoa kutoka kwa adui yangu mwenye nguvu,^c

Kutoka kwa wale wanao-nichukia, waliokuwa na nguvu nyingi kuliko mimi.^d

- 18** Walinikabili katika siku ya msiba wangu,^e

Lakini Yehova alikuwa tegemeo langu.

- 19** Alinitoa nje na kunileta mahali penye usalama;^{*} Aliniokoa kwa sababu alipendezwa nami.^f

- 20** Yehova hunithawabisha kulingana na uadilifu wangu;^g

Hunilipa kulingana na usafi* wa mikonu yangu.^h

- 21** Kwa maana nimezishika njia za Yehova, Nami sijamwacha kwa uovu Mungu wangu.

- 22** Hukumu zake zote ziko mbele yangu; Sitazipuuzwa sheria zake.

- 23** Nitabaki bila lawama mbele zake,ⁱ Nami nitajiepusha na uovu.^j

- 24** Yehova na anilipe kulingana na uadilifu wangu,^k Kulingana na usafi* wa mikonu yangu mbele zake.^l

- 25** Kwa mtu mshikamanifu unatenda kwa ushikamanifu;^m

18:19 *Au "mahali penye nafasi kubwa."
18:20, 24 *Au "ukosefu wa hatia."

- Kwa mtu asiye na lawama unatenda bila lawama;^a
- 26** Kwa walio safi unajidhihirisha mwenyewe kuwa safi.^b
Lakini kwa waliopotoka unajidhihirisha mwenyewe kuwa mwenye busara.^c
- 27** Kwa maana wewe huwao-koa watu wa hali ya chini*^d
Lakini unawashusha wenye kiburi.^e
- 28** Kwa maana ni wewe unayeiywasha taa yangu, Ee Yehova,
Mungu wangu ambaye hulifanya giza langu liangaze.^f
- 29** Kwa msaada wako ninaweza kukabiliana na kundi la wavamizi;^g
Kwa nguvu za Mungu nina-weza kuupanda ukuta.^h
- 30** Njia ya Mungu wa kweli ni kamilifu;ⁱ
Neno la Yehova ni safi.^j
Yeye ni ngao kwa wote wanaomkimbilia.^k
- 31** Kwa maana ni nani aliye Mungu ila Yehova?^l
Na ni nani aliye mwamba isipokuwa Mungu wetu?^m
- 32** Mungu wa kweli ndiye anayenivisha nguvu,ⁿ
Naye ataifanya njia yangu iwe kamilifu.^o
- 33** Huifanya miguu yangu iwe kama ya paa;
Hunifanya nisimame mahali palipo juu.^p
- 34** Huizoeza mikono yangu kupigana vita;
Mikono yangu inaweza kuukunja upinde wa shaba.

18:27 *Au "wanaoteseka." #Tnn., "unayashusha macho ya kiburi."

SURA YA 18

a 2Sa 22:26-31
Ayu 34:11
Yer 32:19

b Mt 5:8

c Zb 125:5

d Ayu 34:28

e Met 6:16, 17
Isa 2:11
Lu 18:14

f Zb 97:11
Isa 42:16

g 2Sa 5:19
Ebr 11:32-34

h 2Sa 22:30
Flp 4:13

i Kum 32:4
Da 4:37
Ufu 15:3

j Zb 12:6
Zb 19:8

k Zb 18:2
Zb 84:11

l Zb 86:8
Isa 45:5

m Kum 32:31
1Sa 2:2
2Sa 22:32-43

n Zb 84:5, 7

o Isa 26:7

p Hab 3:19

Safu ya 2

a Mwa 15:1
Kum 33:29
Zb 28:7

b 2Sa 22:36
Zb 113:6-8

c Zb 17:5

d Zb 2:8, 9

e Zb 44:5

f 2Sa 22:41
Zb 34:21

g 1Sa 30:6

h 2Sa 8:3
Zb 2:8

i 2Sa 22:44-46

- 35** Wewe hunipa ngao yako ya wokovu,^a
Mkono wako wa kuume hunitegemeza,*
Na unyenyekevu wako hunifanya niwe mkuu.^b
- 36** Unapanua njia kwa ajili ya hatua zangu;
Miguu yangu haitateleza.*^c
- 37** Nitawafuatia maadui wangu na kuwapita;
Sitarudi mpaka wataka-poangamizwa kabisa.
- 38** Nitawaponda wasiweze kuinuka;^d
Wataanguka chini ya miguu yangu.
- 39** Utanipa nguvu kwa ajili ya vita;
Utawafanya maadui wangu waanguke chini yangu.^e
- 40** Utawafanya maadui wangu wanikimbie,*
Nami nitawakomesha*^f
wale wanaonichukia.^f
- 41** Wanalilia msaada, lakini hakuna mtu wa kuwaokoa;
Hata wanamlilia Yehova, lakini yeye hawajibu.
- 42** Nitawaponda wawe laini kama mavumbi katika upepo;
Nitawatupa nje kama matope barabarani.
- 43** Utaniokoa kutoka kwa watu wanaotafuta makosa.^g
Utaniweka kuwa kiongozi wa mataifa.^h
Watu ambao siwajui watanitumikia.ⁱ

18:35 *Au "hunidumisha." 18:36 *Au "Vifundo vya miguu yangu havitateleza." 18:40 *Au "Utaniumyesha migo-ngo ya maadui wangu." #Au "nitawaniamazisha."

44 Watanitii watakaposikia fununu tu;

Wageni watakuja wakijikunyaata mbele zangu.^a

45 Wageni watakosa ujasiri;* Watakuja wakitetemeka kutoka katika ngome zao.

46 Yehova yuko hai! Mwamba wangu na asifiwe!^b Mungu wa wokovu wangu na akwezwe.^c

47 Mungu wa kweli hunilipizua kisasi;^d Huyatiisha mataifa chini yangu.

48 Yeye huniokoa kutoka kwa maadui wangu wenye hasira;

Unaniinua juu ya wale wanaonishambulia;^e

Unaniokoa kutoka kwa mtu mkatili.

49 Ndiyo sababu nitakutukua za wewe miongoni mwa mataifa, Ee Yehova,^f Nami nitaliambia sifa* jina lako.^g

50 Yeye hutenda matendo makuu ya wokovu kwa ajili ya mfalme wake;*^h Humtendea mtiwa-mafuta wake kwa upendo mshikamanifu,ⁱ

Kwa Daudi na kwa uzao wake*^j milele.^j

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

19 Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu;^k Na anga lililo juu lina-tangaza kazi ya mikono yake.^l

2 Sikubadua baada ya siku zina-bubujisha maneno yake,

18:45 *Au "watafifia." 18:49 *Au "nitapigiza muziki." 18:50 *Au "humpa ushindi mkubwa mfalme wake." *Tnn., "mbevu yake."

SURA YA 18

a Kum 33:29

b Kum 32:4

c Kut 15:2
2Sa 22:47-49

d Kum 32:35
Nah 1:2
Ro 12:19

e 2Sa 7:9
Zb 59:1

f Kum 32:43
Zb 117:1
Isa 11:10

g 2Sa 22:50, 51
1Nya 16:9
Ro 15:9

h Zb 2:6
Zb 144:10

i 2Sa 7:15-17
1Fa 3:6

j Zb 89:20, 36
Isa 9:7
Lu 1:32, 33
Ufu 5:5

SURA YA 19

k Zb 8:3, 4
Isa 40:22
Ro 1:20

l Zb 150:1
Ufu 4:11

Safu ya 2

a Ro 10:18

b Zb 104:19

c Zb 119:72

d Zb 23:3

e Zb 119:111,
129

f Met 1:5
2Ti 3:15

g 2Nya 24:9, 10

h Met 4:4
Met 6:23
Mt 6:22

i Kum 10:12
Met 1:7
Mal 3:16

j Zb 119:137,
160
Ufu 16:7

Na usiku baada ya usiku zinafunua ujuzi.

3 Hakuna usemi, wala hakuna maneno; Sauti zake hazisikiki.

4 Lakini sauti zake zimefika* katika dunia yote,

Na ujumbe wake umefika mpaka kwenye miisho ya dunia inayokaliwa.^a

Amepiga hema mbinguni kwa ajili ya jua;

5 Ni kama bwana harusi anayetoka katika chumba chake;

Linashangilia kama mwanamume hodari anayekimbia kwenye njia yake.

6 Linachomoza kutoka mwisho mmoja wa mbingu, Nalo huzunguka mpaka mwisho mwingine;^b Na hakuna chochote kinachojificha joto lake.

7 Sheria ya Yehova ni kamilifu,^c hurudisha nguvu.*^d Kikumbusho cha Yehova kinategemeka,^e humfanya asiye na uzoefu awe na hekima.^f

8 Maagizo kutoka kwa Yehova ni ya uadilifu, huufanya moyo ushangilie;^g

Amri ya Yehova ni safi, hu-yafanya macho yang'ae.^h

9 Kumwogopa Yehova ni jambo safi,ⁱ hudumu milele.

Hukumu za Yehova ni za kweli; zote ni za uadilifu.^j

19:4 *Au labda, "kamba yake ya kupimia imefika." 19:7 *Au "huirudisha nafsi."

10 Zinatamanika kuliko dhahabu,
Kuliko dhahabu nyingi bora,*^a

Na tamu zaidi kuliko asali,^b asali inayodondo-
ka kutoka katika sega.

11 Mtumishi wako ameonywa kupitia hizo;^c
Anapozishika anapata thawabu kubwa.^d

12 Ni nani anayeweza kutambua makosa?^e
Nitangaze kuwa sina hatia ya dhambi nisizojua.

13 Na unizuie mimi mtumishi wako nisitende matendo ya kimbelembele;^f
Usiruhusu yanitawale.^g
Ndipo nitakapokuwa kamili,^h

Na sitakuwa na hatia ya dhambi zilizo wazi.*

14 Maneno ya kinywa changu na kutafakari kwa moyo wangu

Na yakupendeze wewe,ⁱ Ee Yehova, Mwamba wangu/na Mkombozi wangu.^k

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

20 Yehova na akujibu katika siku ya taabu.

Jina la Mungu wa Yakobo na likulinde.^l

2 Na akuletee msaada kutoka mahali patakatifu^m
Na kukutegemeza kutoka Sayuni.ⁿ

3 Na akumbuke matoleo yako yote ya zawadi;
Na aikubali kwa upendeleo* dhabihu yako ya kuteketezwa. (*Sela*)

19:10 *Au "iliyosafishwa." 19:13 *Au "dhambi nyingi." 20:3 *Tnn., "aione kuwa mafuta."

SURA YA 19

a Zb 119:127

Met 8:10

b Zb 119:103

Met 16:24

c Zb 119:11

d Zb 119:165

e 1Ko 4:4

f Mwa 20:6

Kum 17:12

1Sa 15:23

2Sa 6:7

2Nya 26:16-18

g Zb 119:133

h Isa 38:3

i Zb 49:3

Zb 51:15

Zb 143:5

Flp 4:8

j Zb 18:2

k Ayu 19:25

Isa 43:14

SURA YA 20

l Zb 9:10

Met 18:10

m 2Nya 20:8, 9

n 2Sa 5:7

Zb 50:2

Zb 134:3

Safu ya 2

a Zb 21:1, 2

b Zb 59:16

c 1Sa 17:45

d Zb 2:2, 4

e Zb 17:7

f Zb 33:17

Isa 31:1

g 2Nya 14:11

2Nya 20:12

2Nya 32:8

h Amu 5:31

Zb 125:1

i Zb 18:50

j Zb 44:4

SURA YA 21

k Zb 63:11

l Zb 28:7

m Zb 2:8

Zb 20:4

4 Na atosheleze tamaa za moyo wako^a
Na kufanikisha mipango yako yote.*

5 Tutapaza sauti kwa shangwe kwa sababu ya matendo yako ya wokovu;^b

Tutainua bendera zetu katika jina la Mungu wetu.^c
Yehova na atimize maombi yako yote.

6 Sasa ninajua kwamba Yehova humwoko mtiwa-mafuta wake.^d
Humjibu kutoka katika mbingu zake takatifu
Kwa wokovu* mkubwa kupitia mkono wake wa kuume.^e

7 Wengine hutegemea magari ya vita na wengine farasi,^f

Lakini sisi tunaliitia jina la Yehova Mungu wetu.^g

8 Wamedondoka na kuanzuka,

Lakini sisi tumeinuka na kurudishwa.^h

9 Ee Yehova, mwokoe mfalme!ⁱ
Atatujibu siku ambayo tutaomba msaada.^j

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

21 Ee Yehova, mfalme hu-shangilia kwa sababu ya nguvu zako;^k

Jinsi anavyoshangilia sana kwa sababu ya matendo yako ya wokovu!^l

2 Umetosheleza tamaa ya moyo wake,^m

Nawe hujamnyima ombi la midomo yake. (*Sela*)

3 Kwa maana unamlaki kwa baraka tele;

20:4 *Au "ushauri wako wote." 20:6 *Au "ushindi."

Unamvika taji la dhahabu bora* kichwani.^a

4 Alikuomba uhai, nawe ukampa,^b

Maisha marefu, * milele na milele.

5 Matendo yako ya wokovu humletea utukufu mkubwa.^c

Unamtunukia adhama na fahari.

6 Unamfanya awe na baraka milele;^d

Unamfanya afurahi kwa shangwe ya kuwa mbele zako.*^e

7 Kwa maana mfalme anamtumaini Yehova;^f

Kwa sababu ya upendo mshikamanifu wa Aliye Juu Zaidi, hatatikiswa kamwe.*^g

8 Mkono wako utawapata maadui wako wote;

Mkono wako wa kuume utawapata wale wanao-kuchukia.

9 Utawafanya wawe kama tanuru lenye moto mkali utakapofika wakati ulioweka wa kuwakazia uangalifu.

Yehova atawameza kwa hasira yake, na moto utawateketeza kabisa.^h

10 Utawaangamiza wazao wao kutoka duniani, Na uzao wao kutoka kati ya wanadamu.

11 Kwa maana walikusudia kukutendea maovu;ⁱ Wamepanga njama ambazo hazitafanikiwa.^j

21:3 *Au "iliyosafishwa." 21:4 *Tnn., "Urefu wa siku." 21:6 *Tnn., "mbele za uso wako." 21:7 *Au "hatapepesuka (hatayumbayumba) kamwe."

SURA YA 21

a 2Sa 12:30

b Zb 13:3
Zb 61:6

c 2Sa 7:8, 9

d Zb 72:17

e Zb 16:11
Zb 45:7

f 1Sa 30:6

g Zb 16:8

h Kum 32:22
Zb 110:5
Mal 4:1

i Zb 34:16

j Zb 2:1

Safu ya 2

a Zb 9:3
Zb 56:9

SURA YA 22

b Zb 22:16
Mt 27:46
Mk 15:34

c Ebr 5:7

d Zb 42:3

e Isa 6:3
1Pe 1:15

f Mwa 15:1, 6

g Kut 14:13
Ebr 11:32-34

h Zb 25:2
Zb 99:6
Ro 10:11

i Zb 31:11
Isa 53:3

12 Kwa maana utawafanya wakimbie^a

Kwa kuwalenga* kwa upinde wako.[#]

13 Inuka, Ee Yehova, katika nguvu zako.

Tutauimbia sifa* uwezo wako.

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa "Paa Jike wa Mapambazuko."* Muziki wa Daudi.

22 Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini ume-niacha?^b

Kwa nini uko mbali usiweze kuniokoa,

Mbali na vilio vyangu vya maumivu makali?^c

2 Mungu wangu, ninaendelea kukuita wakati wa mchana, nawe hunijibu;^d Na wakati wa usiku sinyamazi.

3 Lakini wewe ni mtakatifu,^e Umezungukwa na* sifa za Israeli.

4 Baba zetu walikutumaini wewe;^f

Walikutumaini, nawe ulikuwa ukiwaokoa.^g

5 Walikulilia kwa sauti, wakaokolewa;

Walikutumaini, nao hawakukatishwa tamaa.*^h

6 Lakini mimi ni mnyoo wala si mwanadamu, Ninadhahiwa na wanadamu na kudharauliwa na watu.*ⁱ

21:12 *Tnn., "kulenga nyuso zao."

#Tnn., "kamba zako za upinde." 21:13

*Tnn., "Tutauimbia na kuupigia muziki."

22:Uta *Labda ni sauti au mtindo wa muziki.

22:3 *Au "Umeketi kwenye kiti cha ufalme kati ya (juu ya)."

22:5 *Au "hawakuaibishwa."

22:6 *Au "Mimi ni fedheha kwa wanadamu na ninadharauliwa na watu."

- 7** Wote wanaoniona hunike-jeli;^a
Wanafyonya midomo na kutikisa vichwa vyao kwa dharau;^b
- 8** "Alijikabidhi mwenyewe kwa Yehova. Acha Yeye amwokoe!
Acha Yeye amwokoe, kwa sababu Yeye anampenda sana!"^c
- 9** Wewe ndiye uliyenitoa tumboni,^d
Ni Wewe uliyenifanya nihi-si nikiwa salama kwenye matiti ya mama yangu.
- 10** Nimewekwa chini ya utunzaji wako* tangu nilipozaliwa;
Tangu nilipokuwa katika tumbo la mama yangu, umekuwa Mungu wangu.
- 11** Usikae mbali nami, kwa maana taabu iko karibu^e
Nami sina msaidizi mwingine.^f
- 12** Ng'ombe dume wengi wachanga wananzunguka;^g
Ng'ombe dume wenye nguvu wa Bashani wanazingira.^h
- 13** Wanafungua vinywa vyao wazi dhidi yangu,ⁱ
Kama simba anayenguruma ambaye anararua windo lake vipande-vipande.^j
- 14** Nimemwagwa kama maji; Mifupa yangu yote imeteguka.
Moyo wangu umekuwa kama nta;^k
Unayeyuka katika sehemu zangu za ndani kabisa.^l
- 15** Nguvu zangu zimekauka kama kigae;^m

22:10 *Tnn., "Nimetupwa kwako."

SURA YA 22

a Zb 35:16

b Zb 109:25

c Mt 27:41-43
Lu 23:35, 36

d Zb 71:6
Zb 139:16

e Zb 10:1

f Lu 23:46
Ebr 5:7

g Zb 68:30

h Eze 39:18

i Mt 26:4

j Zb 57:4
1Pe 5:8

k Lu 22:44
Yoh 12:27

l Mt 26:38
Mk 14:33

m Met 17:22

Safu ya 2

a Yoh 19:28

b Isa 53:12
1Ko 15:3, 4

c Zb 59:5, 6
Lu 22:63

d Zb 86:14

e Mt 27:35
Yoh 20:25

f Zb 34:20
Yoh 19:36

g Mk 15:24
Lu 23:34
Yoh 19:23, 24

h Zb 10:1

i Zb 40:13

j Zb 22:16

k Zb 35:17

l Yoh 17:6

m Zb 40:9
Ebr 2:11, 12

n Zb 50:23

Ulimi wangu unashikamana na fizi zangu;^a
Unanishusha chini kwenye mavumbi ya kifo.^b

16 Kwa maana mbwa wananzunguka;^c

Wanazingira kama kundi la watenda maovu,^d

Kama simba, wanaishambulia mikono yangu na miguu yangu.^e

17 Ninaweza kuhesabu mifupa yangu yote.^f

Wananitazama na kunikodolea macho.

18 Wanagawana mavazi yangu,

Nao wanalipigia kura vazi langu.^g

19 Lakini wewe, Ee Yehova, usiendeleo kukaa mbali.^h

Wewe ni nguvu zangu; njoo haraka unisaidie.ⁱ

20 Niokoe* kutoka kwa upanga,

Uhai wangu wenye thamani[#] kutoka katika makucha ya[^] mbwa;^j

21 Niokoe kutoka katika kinywa cha simba^k na pembe za ng'ombe dume wa mwituni;

Nijibu na uniokoe.

22 Nitalitangaza jina lako kwa ndugu zangu;^l

Katikati ya kutaniko nitakusifu.^m

23 Ninyi mnaomwogopa Yehova, msifuni!

Enyi nyote uzao wa* Yakobo, mtukuzeni!ⁿ

Mwogopeni yeye, enyi nyote uzao wa[#] Israeli.

22:20 *Au "lokoe nafsi yangu." [#]Tnn., "Uhai pekee nilio nao," yaani, nafsi yake. [^]Tnn., "mkono wa." 22:23 *Tnn., "mbegu ya." [#]Tnn., "mbegu ya."

- 24** Kwa maana hajadharau wala kuchukizwa na mateso ya yule anayekandamizwa;^a Hajauficha uso wake kutoka kwake.^b Alipomlilia amsaidie, alisikia.^c
- 25** Nitakusifu katika kutaniko kubwa;^d Nitatimiza nadhiri zangu mbele ya wale wanaomwogopa.
- 26** Wapole watakula na kushiba;^e Wale wanaomtafuta Yehova watamsifu.^f Na ufurahie maisha* milele.
- 27** Miisho yote ya dunia itakumbuka na kumgeukia Yehova. Familia zote za mataifa zitainama chini mbele zako.^g
- 28** Kwa maana ufalme ni wa Yehova;^h Anayatawala mataifa.
- 29** Watu wote wenye ufanisi* duniani watakula na kumwinamia; Wote wanaoshuka mavumbini watapiga magoti mbele zake; Hakuna yeyote kati yao anayeweza kuokoa uhai wao.[#]
- 30** Wazao wao watamtu-mikia;* Kizazi kitakachokuja kitaambiwa kumhusu Yehova.
- 31** Watakuja na kusimulia uadilifu wake. Watawaambia watu ambao

22:26 *Tnn., "Moyo wako na uishi."
 22:29 *Tnn., "wanene." #Au "nafsi zao."
 22:30 *Tnn., "Mbegu itamtumikia."

SURA YA 22

a Zb 34:6
 Zb 69:33
 b Hes 6:25
 c Ebr 5:7
 d Zb 35:18
 Zb 40:10
 Zb 111:1
 e Zb 37:11
 Isa 65:13
 f Sef 2:3
 g Mwa 22:18
 Ufu 7:9
 Ufu 15:4
 h 1Nya 29:11
 Ufu 11:17

Safu ya 2

SURA YA 23

a Zb 80:1
 Yer 23:3
 Eze 34:12
 1Pe 2:25
 b Zb 34:9
 Zb 84:11
 Mt 6:33
 Flp 4:19
 Ebr 13:5
 c Eze 34:13, 14
 d Zb 19:7
 Zb 51:12
 e Zb 31:3
 f Ayu 38:17
 g Zb 3:6
 Zb 27:1
 Isa 41:10
 h Isa 43:2
 Ro 8:31
 i Zb 22:26
 Zb 31:19
 j Lu 7:46
 Yak 5:14
 k Zb 16:5
 l Zb 103:17
 m Zb 15:1-5
 Zb 27:4
 Zb 65:4
 Zb 122:1

SURA YA 24

n 1Nya 29:11
 Ayu 41:11
 1Ko 10:26
 o Mwa 1:9
 Ayu 38:11
 Zb 136:6
 Yer 5:22

bado hawajazaliwa mambo aliyofanya.

Muziki wa Daudi.

- 23** Yehova ni Mchungaji wangu.^a Sitakosa chochote.^b
- 2** Hunilaza katika malisho yenye majani mengi; Huniongoza kwenye sehemu za kupumzika zenye maji mengi.^{*c}
- 3** Huniburudisha.^{*d} Huniongoza katika njia za[#] uadilifu kwa ajili ya jina lake.^e
- 4** Hata nikitembea katika bonde lenye kivuli kizito,^f Siogopi madhara yoyote,^g Kwa maana wewe uko pamoja nami;^h Fimbo yako na gongo lako hunipa uhakika.*
- 5** Wewe huniandalia meza mbele ya maadui wangu.ⁱ Unakiburudisha* kichwa changu kwa mafuta;^j Kikombe changu kimejaza vizuri.^k
- 6** Kwa hakika wema na upendo mshikamanifu utanifuatia sikuzote za maisha yangu,^l Nami nitakaa katika nyumba ya Yehova siku zangu zote.^m
- Muziki wa Daudi.
- 24** Dunia na vyote vilivyo-mo ni vya Yehova,ⁿ Nchi inayozaa na wale wanaokaa ndani yake.
- 2** Kwa maana ameiweka imara kabisa juu ya bahari^o

23:2 *Au labda, "maji matulivu." 23:3 *Au "Huiburudisha nafsi yangu."
 #Tnn., "mapito ya; vijia vya." 23:4 *Au "hunifariji." 23:5 *Au "Unakipaka."

Na kuiweka imara kabisa juu ya mito.

- 3 Ni nani anayeweza kuupanda mlima wa Yehova,^a

Na ni nani anayeweza kusimama mahali pake patakatifu?

- 4 Yeyote mwenye mikono isiyo na hatia na mwenye moyo safi,^b

Ambaye hajaapa kwa uwongo kwa uhai Wangu,* Wala kuapa kwa udanganifu.^c

- 5 Atapokea baraka kutoka kwa Yehova^d

Na uadilifu* kutoka kwa Mungu wa wokovu wake.^e

- 6 Hiki ndicho kizazi cha wale wanaomtafuta, Cha wale wanaoutafuta uso wako, Ee Mungu wa Yakobo. (*Sela*)

- 7 Inueni vichwa vyenu, enyi malango;^f

Fungukeni,* enyi milango ya kale, Ili Mfalme mtukufu aingie!^g

- 8 Mfalme huyu mtukufu ni nani?

Yehova, mwenye nguvu na hodari,^h

Yehova, hodari katika vita.ⁱ

- 9 Inueni vichwa vyenu, enyi malango;^j

Fungukeni, enyi milango ya kale, Ili Mfalme mtukufu aingie!

- 10 Mfalme huyu mtukufu ni nani?

Yehova wa majeshi—yeye ndiye Mfalme mtukufu.^k (*Sela*)

24:4 *Au “nafsi Yangu,” ikirejelea mtu kuapa kwa uhai wa Yehova. 24:5 *Au “haki.” 24:7 *Au “Inukeni.”

SURA YA 24

a Zb 15:1-5

b 2Sa 22:21
Isa 33:15, 16
Mt 5:8

c Zb 34:12, 13
Mal 3:5

d Zb 128:1-5

e Isa 12:2

f Zb 118:19
Zb 122:2

g 2Sa 6:15
Zb 48:1-3

h Zb 93:1

i Kut 15:3
1Sa 17:47
2Nya 20:15
Isa 42:13

j Zb 118:19

k 1Nya 29:11

Safu ya 2

SURA YA 25

a Isa 26:3

b Ro 10:11

c Zb 41:11

d Zb 69:6

e Zb 31:17

f Kut 33:13
Zb 86:11
Zb 143:8

g Zb 27:11

h Zb 43:3

i Kut 34:6
Isa 55:3

j Zb 103:17
Zb 136:1

k Zb 6:4

Zb 51:1

l Kut 33:19
Zb 27:13

Wa Daudi.

✠ [Aleph]

25 Nakugeukia wewe,* Ee Yehova.

‡ [Beth]

- 2 Mungu wangu, ninakutumaini wewe;^a

Usiruhusu niabishwe.^b

Usiruhusu maadui wangu wanicheke.^c

‡ [Gimel]

- 3 Kwa hakika hakuna yeyote anayekutumaini atakayeabishwa,^d

Lakini aibu inawangoja wale wanaotenda kwa hila bila sababu.^e

‡ [Daleth]

- 4 Nijulishe njia zako, Ee Yehova;^f

Nifundishe vijia vyako.^g

‡ [He]

- 5 Nitembeze katika kweli yako na kunifundisha,^h Kwa maana wewe ni Mungu wa wokovu wangu.

† [Waw]

Ninakutumaini mchana kutwa.

† [Zayin]

- 6 Kumbuka rehema zako, Ee Yehova, na upendo wako mshikamanifu,ⁱ

Ambazo umedhihirisha sikuzote.*^j

‡ [Heth]

- 7 Usikumbuke dhambi na makosa niliyotenda nilipokuwa kijana.

Nikumbuke kulingana na upendo wako mshikamanifu,^k

Kwa ajili ya wema wako, Ee Yehova.^l

25:1 *Au “Nainua nafsi yangu kwako.”

25:6 *Au “Ambazo ni za tangu nyakati za kale.”

ⲛ [Teth]

8 Yehova ni mwema na mnyoofu.^a

Ndiyo sababu yeye huwafundisha watenda dhambi njia wanayopaswa kuishi.^b

* [Yod]

9 Atawaongoza wapole katika yaliyo sawa,^{*c}

Naye atawafundisha wapole njia yake.^d

ⲓ [Kaph]

10 Njia zote za Yehova ni upe-
ndo mshikamanifu na uaminifu

Kwa wale wanaoshika agano lake^e na vikumbusho vyake.^f

ⲛ [Lamed]

11 Kwa ajili ya jina lako, Ee Yehova,^g

Nisamehe kosa langu, ingawa ni kubwa.

ⲛ [Mem]

12 Ni nani anayemwogopa Yehova?^h

Atamfundisha kuhusu njia anayopaswa kuchagua.ⁱ

ⲓ [Nun]

13 Atajionea* yaliyo mema,^j Na wazao wake wataimiliki* dunia.^k

ⲓ [Samekh]

14 Urafiki wa karibu pamoja na Yehova ni wa wale wanaomwogopa,^l Naye huwajulisha agano lake.^m

ⲛ [Ayin]

15 Macho yangu humtazama Yehova daima,ⁿ

Kwa maana ataiweka huru miguu yangu kutoka katika wavu.^o

SURA YA 25

a Zb 92:15
Zb 119:68
Zb 145:9
Mdo 14:17

b Zb 119:33
Isa 30:20
Mik 4:2

c Sef 2:3

d Zb 32:8

e Kum 29:1

f Zb 19:7

g Zb 31:3
Zb 79:9
Zb 109:21
Zb 143:11
Eze 36:22
Da 9:19
Mt 6:9

h Zb 111:10

i Zb 37:23

j Zb 31:19

k Zb 37:11

l Met 3:32
Yoh 15:15

m Mwa 18:17
Mwa 22:17
Amo 3:7

n Zb 141:8

o Zb 91:3
Zb 124:6-8

Safu ya 2

a Zb 73:21

b 2Sa 16:12

c Zb 32:5
Zb 51:9

d Zb 17:8
Zb 121:7

e Zb 41:12

f Zb 37:34

SURA YA 26

g 2Fa 20:3

h Zb 21:7

i Zb 17:3
Zb 66:10

ⲛ [Pe]

16 Nielekezee uso wako na kunionyesha kibali, Kwa maana niko peke yangu na sina uwezo.

ⲛ [Tsade]

17 Taabu za moyo wangu zimeongezeka;^a Niondolee maumivu yangu makali.

ⲛ [Resh]

18 Yaone mateso yangu na shida yangu,^b Nawe unisamehe dhambi zangu zote.^c

19 Tazama jinsi maadui wangu walivyo wengi Na jinsi wanavyonichukia vikali.

ⲛ [Shin]

20 Ulinde uhai wangu* na uniokoe.^d Usiruhusu niaibishwe, kwa maana nimekukimbilia wewe.

ⲛ [Taw]

21 Utimilifu na unyoofu na vinilinde,^e Kwa maana ninakutumaini wewe.^f

22 Ee Mungu, mwokoe* Israeli kutoka katika taabu zake zote.

Wa Daudi.

26 Unihukumu, Ee Yehova, kwa maana nimetembea katika utimilifu wangu;^g

Nimemtumaini Yehova bila kuyumbayumba.^h

2 Nichunguze, Ee Yehova, na unijaribu; Safisha mawazo yangu ya ndani kabisa* na pia moyo wangu.ⁱ

25:9 *Tnn., "katika hukumu." 25:13 *Au "Nafsi yake itajionea." *Tnn., "mbegu yake itamiliki."

25:20 *Au "Ilinde nafsi yangu." 25:22 *Tnn., "mkombwe." 26:2 *Au "hisia zangu za ndani kabisa." *Tnn., "figo zangu."

- 3** Kwa maana upendo wako mshikamanifu uko mbele yangu daima, Nami ninatembea katika kweli yako.^a
- 4** Sishirikiani* na watu wadanganyifu,^b Nami huwaepuka wale wanaoficha jinsi walivyo.[#]
- 5** Ninachukia kundi la wao-vu,^c Nami ninakataa kushirikiana* na waovu.^d
- 6** Nitanawa mikono yangu katika ukosefu wa hatia, Nami nitapiga mwendo kuzunguka madhabahu yako, Ee Yehova,
- 7** Ili niifanye sauti ya utoaji shukrani isikike^e Na kutangaza kazi zako zote zinazostaajibisha.
- 8** Yehova, ninaipenda nyumba ambamo unakaa,^f Mahali ambapo utukufu wako hukaa.^g
- 9** Usinifagilie mbali* pamoja na watenda dhambi^h Wala kuniuma pamoja na watu wakatili,[#]
- 10** Ambao mikono yao hute nda matendo ya* aibu, Na ambao mkono wao wa kulia umejaa rushwa.
- 11** Lakini mimi, nitatembea katika utimilifu wangu. Niokoe* na kunionyesha kibali.
- 12** Mguu wangu umesimama mahali tambarare;ⁱ Katika kutaniko kubwa,* nitamsifu Yehova.^j

26:4 *Tnn., "Siketi." #Au "sichangamani na wanafiki." 26:5 *Tnn., "kuketi." 26:9 *Tnn., "Usiifagilie mbali nafsi yangu." #Au "watu wanaomwaga damu." 26:10 *Au "mwenendo wa." 26:11 *Tnn., "Nikomboe." 26:12 *Tnn., "makusanyiko."

SURA YA 26

a Zb 43:3

Zb 86:11

b Yer 15:17

c Zb 139:21

d Zb 1:1

e Zb 50:23

Zb 95:2

f 1Sa 3:3

1Nya 16:1

Zb 27:4

g Zb 63:2

h 1Sa 25:29

i 1Sa 2:9

Met 10:9

j Zb 111:1

Safu ya 2

SURA YA 27

a Zb 36:9

Zb 43:3

Zb 119:105

b Zb 23:4

Ro 8:31

Ebr 13:6

c Zb 62:6

Isa 12:2

d Zb 22:16

e 2Nya 20:15

2Nya 32:7

Zb 3:6

f Zb 23:6

Zb 65:4

g 1Sa 3:3

1Nya 16:1

Zb 26:8

h Zb 32:7

Zb 57:1

Sef 2:3

i Zb 61:4

j Zb 40:2

Wa Daudi.

27 Yehova ni nuru yangu^a na wokovu wangu.

Nimwogope nani?^b

Yehova ni ngome ya uhai wangu.^c

Nimhofu nani?

2 Waovu waliponishambulia ili waunyafue mwili wangu,^d

Wapinzani wangu na maadui wangu ndio waliojikwaa na kuanguka.

3 Hata jeshi likipiga kambi ili kunishambulia,

Moyo wangu hautaogopa.^e

Hata vita vikizuka dhidi yangu,

Bado nitaendelea kuwa jasiri.

4 Nimemwomba Yehova jambo moja

—Ndilo nitakalolitafuta—

Kwamba nikae katika nyumba ya Yehova sikuzote za maisha yangu,^f

Ili kuutazama uzuri wa Yehova

Na kutazama kwa uthamini* hekalu lake.^{#g}

5 Kwa maana atanificha katika banda lake siku ya msiba;^h

Atanificha mahali pa siri katika hema lake;ⁱ

Ataniweka juu kwenye mwamba.^j

6 Sasa kichwa changu kiko juu sana ya maadui wangu wanaonizingira;

Nitatoa dhabihu katika hema lake kwa kelele za shangwe;

Nitamwimbua sifa* Yehova.

27:4 *Au "kutazama kwa kutafakari."

#Au "mahali pake patakatifu." 27:6 *Au "Nitampigia muziki."

- 7 Nisikie, Ee Yehova, nina-polia kwa sauti;^a
Nionyeshe kibali na kuni-jibu.^b
- 8 Moyo wangu umesema hivi kwa niaba yako: “Utafute uso wangu.” Nitautafuta uso wako, Ee Yehova.^c
- 9 Usinifiche uso wako.^d Usimfukuze kwa hasira mtumishi wako. Wewe ni msaidizi wangu;^e Usinitupe wala usiniache, Mungu wa wokovu wangu.
- 10 Hata baba yangu na mama yangu wakiniacha,^f Yehova mwenyewe atanichukua.^g
- 11 Nifundishe njia yako, Ee Yehova,^h Niongoze katika kijia cha unyoofu kwa sababu ya maadui wangu.
- 12 Usinitie mikononi mwa maadui wangu,ⁱ Kwa maana mashahidi wa uwongo wameinuka dhidi yangu,^j Nao wanatoa vitisho vya kunitendea kwa ukatili.
- 13 Ninge kuwa wapi ikiwa singekuwa na imani Kwamba nitauona wema wa Yehova katika nchi ya walio hai?^{*k}
- 14 Mtumaini Yehova;^l Uwe jasiri na uwe na moyo mkuu.^m Naam, mtumaini Yehova. Wa Daudi.
- 28** Ninaendelea kukulilia wewe, Ee Yehova Mwamba wangu;ⁿ

27:13 *Au labda, “Kwa hakika nina imani kwamba nitauona wema wa Yehova katika nchi ya walio hai.”

SURA YA 27

a Zb 130:2

b Zb 4:1
Zb 5:2c Zb 63:1
Zb 105:4
Sef 2:3d Zb 69:17
Zb 143:7

e Zb 46:1

f Zb 69:8

g Isa 49:15

h Zb 25:4
Zb 86:11
Isa 30:20
Isa 54:13i Zb 31:8
Zb 41:2
Zb 41:11

j Mt 26:59-61

k Ayu 33:28-30

l Zb 25:3
Zb 62:5

m Isa 40:31

SURA YA 28

n Kum 32:4
Isa 26:4

Safu ya 2

a Ayu 33:28

b Zb 5:7

c Hes 16:25, 26
Zb 26:9

d Zb 62:4

e Zb 59:12
Yer 18:22f Zb 62:12
2Th 1:6

g Ayu 34:26, 27

h Isa 5:12

i Isa 12:2

j Mwa 15:1
2Sa 22:3
Zb 3:3

k Zb 56:4

- Usiwe kama kiziwi kwangu.
Ukininyamazia,
Nitakuwa kama wale wanaoshuka shimoni.^{*a}
- 2 Sikia sihi zangu ninapokulilia unisaidie
Ninapoinua mikono yangu kuelekea chumba cha ndani zaidi cha mahali pako patakatifu.^b
- 3 Usinikokote pamoja na waovu, pamoja na wale wanaotenda mambo yanayodhuru,^c Wale wanaoongea na jirani yao maneno ya amani lakini uovu uko mioyoni mwao.^d
- 4 Walipe kulingana na mate-ndo yao,^e Kulingana na mazoea yao maovu. Walipe kulingana na kazi ya mikono yao, Kulingana na mambo waliyotenda.^f
- 5 Kwa maana hawazingatii utendaji wa Yehova,^g Wala kazi ya mikono yake.^h Atawabomoa kabisa naye hatawajenga.
- 6 Yehova na asifiwe, Kwa maana amesikia sihi zangu za kuomba msaada.
- 7 Yehova ni nguvu zanguⁱ na ngao yangu;^j Moyo wangu unamtumaini yeye.^k Amenisaidia, na moyo wangu unashangilia, Kwa hiyo nitamsifu kwa wimbo wangu.
- 8 Yehova ni nguvu kwa watu wake;

28:1 *Au “kaburini.”

Yeye ni ngome, anamletea mtiwa-mafuta wake wokovu mkubwa.^a

- 9 Waokoe watu wako, na uubariki urithi wako.^b
Wachunge na kuwabeba mikononi mwako milele.^c

Muziki wa Daudi.

- 29** Mpeni Yehova anachostahili, enyi wana wa watu hodari,

Mpeni Yehova anachostahili kwa sababu ya utukufu wake na nguvu zake.^d

- 2 Mpeni Yehova utukufu ambao jina lake linastahili.

Mwinamieni* Yehova katika mapambo matakatifu.[#]

- 3 Sauti ya Yehova husikika juu ya maji;
Mungu mtukufu hunguruma.^e
Yehova yuko juu ya maji mengi.^f

- 4 Sauti ya Yehova ina nguvu;^g
Sauti ya Yehova ina fahari.

- 5 Sauti ya Yehova inavunja mierezi;
Naam, Yehova anaipasua pasua mierezi ya Lebanoni.^h

- 6 Hufanya Lebanoni* iruke-ruke kama ndama, Na Sirioni' kama ng'ombe dume mchanga wa mwituni.

- 7 Sauti ya Yehova hupiga kwa miali ya moto;^j

- 8 Sauti ya Yehova huifanya nyika itetemeke,^k

29:2 *Au "Mwabuduni." #Au labda, "kwa sababu ya fahari ya utakatifu wake." 29:6 *Inaonekana ni safu ya milima ya Lebanoni.

SURA YA 28

a 1Sa 16:13
2Sa 22:3
Zb 20:6

b Kum 9:29

c Isa 40:11

SURA YA 29

d 1Nya 16:28, 29

e 1Sa 7:10
Zb 18:13

f Zb 104:3

g Ayu 26:11
Ayu 40:9

h Isa 2:12, 13

i Kum 3:8, 9

j Kut 19:18
Zb 77:18

k Isa 13:13
Ebr 12:26

Safu ya 2

a Hes 13:26

b Isa 10:17, 18
Eze 20:47

c Ayu 38:25

d 1Ti 1:17

e Isa 40:29

f Zb 72:7

SURA YA 30

g Zb 25:2
Zb 41:11

h 2Fa 20:5
Zb 6:2
Zb 103:3

i Zb 86:13

j Zb 16:10
Zb 28:1
Isa 38:17
Yon 2:6

k Zb 32:11

l Kut 3:15

m Isa 12:1

Yehova huifanya nyika ya Kadeshi^a itetemeke.

- 9 Sauti ya Yehova humfanya paa atetemeke na kuzaa Nayo huivua kabisa misitu.^b

Na wote walio katika hekalu lake husema: "Utukufu!"

- 10 Yehova huketi kwenye kiti cha ufalme juu ya mafuriko ya maji;^{*c}

Yehova huketi kwenye kiti cha ufalme akiwa Mfalme milele.^d

- 11 Yehova atawapa nguvu watu wake.^e

Yehova atawabariki watu wake kwa amani.^f

Muziki. Wimbo wa kuizindua nyumba. Wa Daudi.

- 30** Nitakukweza, Ee Yehova, kwa maana umeniinua* juu;

Hukuruhusu maadui wangu washangilie juu yangu.^g

- 2 Ee Yehova Mungu wangu, nilikulilia unisaidie, nawe ukaniponya.^h

- 3 Ee Yehova, umeniinua* kutoka Kaburini.^{#i}

Ulifanya niendeleo kuwa hai; uliniokoa nisizame shimoni.^{Δj}

- 4 Mwimbieni sifa* Yehova, enyi washikamanifu wake,^k

Lishukuruni jina lake takatifu;^{#l}

- 5 Kwa sababu hasira yake ni ya muda mfupi tu,^m

29:10 *Au "bahari ya mbinguni." 30:1 *Au "umenivuta." 30:3 *Au "umeiinua nafsi yangu." #Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. ΔAu "kaburini." 30:4 *Au "Mpigieni muziki." #Tnn., "Ushukuruni ukumbusho wake."

Lakini kibali chake* hudumu maisha yote.^a

Huenda kukawa na kilio jioni, lakini asubuhi, kuna kilio cha shangwe.^b

6 Nilipokuwa na amani, nilisema:
"Sitatikiswa kamwe."*

7 Ee Yehova, nilipokuwa na kibali chako,* ulinifanya niwe imara kama mlima.^c

Lakini ulipouficha uso wako, niliogopa.^d

8 Niliendelea kukulilia wewe, Ee Yehova;^e
Nami niliendelea kukusihi wewe, Ee Yehova, unio-nyeshe kibali.

9 Kuna faida gani nikifa,* nikishuka shimoni?^f
Je, mavumbi yatakusifu?^g
Je, yatasimulia kuhusu uaminifu wako?^h

10 Sikia, Ee Yehova, na unio-nyeshe kibali.ⁱ
Ee Yehova, uwe msaidizi wangu.^j

11 Umehadili maombolezo yangu kuwa dansi;
Umenivua nguo zangu za magunia, nawe unanivisha shangwe,

12 Ili niimbe* sifa yako, nisinyamaze.
Ee Yehova Mungu wangu, nitakusifu milele.

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

31 Nimekukimbilia wewe, Ee Yehova.^k
Acha nisiaibishwe kamwe.^l
Niokoe kwa sababu ya uadilifu wako.^m

30:5 *Au "nia yake njema." 30:6 *Au "Sitapepesuka (sitayumbayumba) kamwe." 30:7 *Au "nia yako njema." 30:9 *Tnn., "Damu yangu ina faida gani." #Au "kaburini." 30:12 *Au "Ili utukufu wangu uimbe."

SURA YA 30

a Isa 54:8

b Zb 126:5

c 2Sa 5:12
Zb 89:17

d Zb 10:1
Zb 143:7

e Zb 34:6
Zb 77:1

f Zb 28:1

g Zb 6:5
Zb 115:17
Mhu 9:10

h Zb 88:11
Isa 38:18

i Zb 143:1

j Zb 28:7

SURA YA 31

k Zb 18:2

l Zb 22:4, 5
Ro 10:11

m Zb 143:1

Safu ya 2

a Zb 40:17
Zb 70:1
Zb 71:2

b 2Sa 22:3
Zb 18:2

c 2Sa 22:2

d Zb 25:11
Yer 14:7

e Zb 23:3

f Zb 91:3
Mt 6:13

g Met 18:10

h Lu 23:46
Mdo 7:59

i Kum 32:4

j Zb 9:13

k Zb 6:7

l Zb 22:14

m Met 15:13

2 Nitegee sikio lako.*
Njoo haraka uniokoe.^a
Uwe kwangu mlima ambao ni ngome,

Ngome ya kuniokoa.^b

3 Kwa maana wewe ni jabali langu na ngome yangu;^c
Kwa ajili ya jina lako,^d
utaniongoza na kunielekeza.^e

4 Utanitoa katika wavu walionitegea kwa siri,^f
Kwa maana wewe ni ngome yangu.^g

5 Naiweka roho yangu mikononi mwako.^h
Umenikombo, Ee Yehova, Mungu wa ukweli.*ⁱ

6 Ninawachukia wale wanaoabudu sanamu zisizo na faida, za ubatili,
Lakini mimi, ninamtumaini Yehova.

7 Nitashangilia sana kwa sababu ya upendo wako mshikamanifu,
Kwa maana umeona dhiki yangu;^j
Unajua mateso makali yaliyo ndani yangu.*

8 Hujanitia mikononi mwa adui,
Lakini unanifanya nisimame mahali salama.*

9 Nionyeshe kibali, Ee Yehova, kwa maana niko katika dhiki.
Maumivu makali yamefanya macho yangu yadhoofike,^k na pia mwili wangu wote.*^l

10 Maisha yangu yamejaa huzuni.^m

31:2 *Au "Inama chini na unisikilize."

31:5 *Au "Mungu mwaminifu." 31:7 *Au "mateso ya nafsi yangu." 31:8 *Au "penye nafasi kubwa." 31:9 *Au "nafsi yangu na tumbo langu."

Na miaka yangu kilio cha maumivu makali.^a

Nguvu zangu zinapungua kwa sababu ya dhambi yangu;

Mifupa yangu inadhoo-fika.^b

11 Ninadhihakiwa na maadui wangu wote.^c

Hasa majirani wangu.

Na rafiki zangu wananio-gopa;

Wanaponiona hadharani, wananikimbia.^d

12 Wameniondoa moyoni* mwao na kunisahau, kana kwamba nimekufa; Mimi ni kama gudulia lili-lovunjika.

13 Nimesikia uvumi mwingi wa uovu;

Nimezungukwa na hofu.^e

Wanapokusanyika pamoja kama kitu kimoja dhidi yangu,

Wanapanga njama ya kuniua.^{*f}

14 Lakini ninakutumaini wewe, Ee Yehova.^g

Ninatangaza: "Wewe ni Mungu wangu."^h

15 Siku* zangu zimo mkono-ni mwako.

Niokoe kutoka mikononi mwa maadui wangu na kutoka kwa wale wanaonitesa.ⁱ

16 Ifanye nuru ya uso wako imwangazie mtumishi wako.^j

Niokoe kwa upendo wako mshikamanifu.

17 Ee Yehova, naomba nisi-aibishwe ninapokulilia wewe.^k

SURA YA 31

a Zb 71:9

b Zb 32:3
Zb 102:3, 5

c Zb 22:6
Zb 42:10
Zb 102:8

d Zb 38:11

e Yer 20:10

f Zb 57:4

g Zb 56:4

h Zb 43:5

i Zb 142:6

j Hes 6:25

k Zb 25:2
Isa 50:7

Safu ya 2

a Ne 6:16
Isa 41:11
Yer 20:11

b 1Sa 2:9

c Zb 12:3
Zb 63:11

d Zb 73:1
Isa 63:7

e Isa 64:4
1Ko 2:9

f Zb 126:2
Isa 26:12

g Zb 27:5
Zb 32:7

h Zb 64:2, 3

i Zb 17:7

j 1Sa 23:7

k Yon 2:4

l 2Nya 33:13
Zb 6:9
Met 15:29
Ebr 5:7

m Kum 10:12

n 1Sa 2:9

Zb 145:20

Waovu na waaibishwe;^a

Na wanyamazishwe Kabu-rini.^{*b}

18 Midomo inayosema uwongo na iwe bubu,^c

Midomo inayoongea kwa kiburi dhidi ya mwadilifu, kwa majivuno na dharau.

19 Jinsi wema wako ulivyo mwingi sana!^d

Umewahifadhia wale wanaokuogopa,^e

Nawe umeuonyesha mbele ya wanadamu wote, kwa niaba ya wale wanaokukimbilia wewe.^f

20 Utawaficha mahali pa siri mbele zako.*^g

Mbali na njama za wana-damu;

Utawaficha katika banda lako

Dhidi ya mashambulizi ya watu wenye nia mbaya.^{#h}

21 Yehova na asifiwe, Kwa maana kwa njia yenye kustaaajibisha, amenionyesha upendo wake mshikamanifuⁱ katika jiji lililozingirwa.^j

22 Lakini mimi nilishikwa na wasiwasi nikasema: "Nitaangamia kutoka mbele zako."^k

Lakini ulisikia sihi zangu za kuomba msaada nilipokulilia kwa sauti.^l

23 Mpendeni Yehova, enyi nyote mlio washikamanifu kwake!^m

Yehova huwalinda waaminifu,ⁿ

Lakini humlipa vilivyo

31:17 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. **31:20** *Au "katika uwepo wako." #Tnn., "Kutoka kwa ugomvi wa ndimi."

31:12 *Au "akilini." **31:13** *Au "kuiondoa nafsi yangu." **31:15** *Tnn., "Nya-kati."

yeyote anayeonyesha kiburi.^a

- 24 Iweni jasiri, na muwe na moyo mkuu,^b
Ninyi nyote mnaomngojea Yehova.^c

Wa Daudi. Maskili.*

- 32** Mwenye furaha ni mtu ambaye amesamehe wa kosa lake, ambaye dhambi yake imefuni kwa.*^d

- 2 Mwenye furaha ni mtu ambaye Yehova hamwoni kuwa mwenye hatia,^e Asiye na udanganyifu katika roho yake.

- 3 Niliponyamaza, mifupa yangu ilidhoofika kwa sababu ya kulia kwa maumivu makali mchana kutwa.^f

- 4 Kwa maana usiku na mchana mkono wako ulinilemea.*^g

Nguvu zangu zilitoweka^h kama mvuke katika joto kavu la kiangazi. (*Sela*)

- 5 Mwishowe nikaungama dhambi yangu kwako; Sikufunika kosa langu.^h Nilisema: "Nitaungama makosa yangu kwa Yehova."ⁱ

Nawe ukanisamehe kosa la dhambi zangu.^j (*Sela*)

- 6 Ndiyo sababu kila mtu aliye mshikamanifu atasali kwako^k

Maadamu unapatikana.^l

Ndipo hata mafuriko haya-tamfikia.

- 7 Wewe ni mahali pangu pa kujificha;

32:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.
32:1 *Au "imesamehewa." 32:4 *Au "hasira yako ilinilemea." #Au "Unyevu-nyevu wa uhai wangu ulibadilika."

SURA YA 31

a 2Sa 22:28
Isa 2:11
Yak 4:6

b Isa 35:4

c Zb 62:1
Omb 3:20, 21
Mik 7:7

SURA YA 32

d Isa 1:18
Mdo 3:19

e Ro 4:7, 8

f Met 28:13

g Zb 38:2

h Zb 38:18
Zb 51:4
1Yo 1:9

i Law 5:5
Zb 41:4

j 2Sa 12:13
Zb 86:5
Zb 103:3
Isa 44:22

k Zb 65:2, 3

l Zb 69:13
Isa 55:6

Safu ya 2

a Zb 9:9

b Kut 15:1
2Sa 22:1

c Zb 86:11

d Met 3:6

e Met 26:3
Yer 8:6

f Zb 34:8
Met 13:21
Met 16:20

SURA YA 33

g Flp 4:4

h Zb 40:3
Zb 98:1
Zb 149:1
Isa 42:10
Ufu 5:9

i Zb 12:6

Utanilinda nisipatwe na taabu.^a

Utanzunguka kwa kelele za shangwe za ukombozi.^b (*Sela*)

- 8 "Nitakupa ufahamu na kukufundisha njia unayopaswa kufuata.^c

Nitakupa ushauri jicho langu likikutazama.^d

- 9 Usiwe kama farasi au nyumbu, asiye na uelewaji,^e Ambaye ni lazima msimko wake udhibitiwe kwa hatamu au lijamu Kabla hajakukaribia."

- 10 Mwovu ana maumivu mengine;

Lakini mtu anayemtumaini Yehova amezungukwa na upendo Wake mshikamanifu.^f

- 11 Furahini kwa sababu ya Yehova na kushangilia, enyi waadilifu;

Pazeni sauti kwa shangwe, ninyi nyote mlilo wanyoofu moyoni.

- 33** Pazeni sauti kwa shangwe, enyi waadilifu, kwa sababu ya Yehova.^g

Ni jambo linalofaa kwa wanyoofu kumsifu yeye.

- 2 Mshukuruni Yehova kwa kinubi;

Mwimbieni sifa* kwa kinanda chenye nyuzi kumi.

- 3 Mwimbieni wimbo mpya;^h Pigeni nyuzi kwa ustadi, na kupaza sauti kwa shangwe.

- 4 Kwa maana neno la Yehova limenyooka,ⁱ

Na kila jambo analofanya linategemeka.

33:2 *Au "Mpigieni muziki."

- 5 Anapenda uadilifu na haki.^a
Dunia imejaa upendo mshikamanifu wa Yehova.^b
- 6 Kwa neno la Yehova mbingu ziliumbwa,^c
Na kwa roho ya* kinywa chake kila kitu kilichomo kiliumbwa.[#]
- 7 Huyakusanya maji ya bahari kana kwamba ni bwawa;^d
Huyaweka mawimbi makubwa ya maji katika maghala.
- 8 Dunia yote na imwogope Yehova.^e
Wakaaji wa nchi* na wamhofu.
- 9 Kwa maana alisema, ikawa;^f
Aliamuru, ikasimama imara.^g
- 10 Yehova amevuruga njama za* mataifa;^h
Ameharibu mipango[#] ya mataifa.ⁱ
- 11 Lakini maamuzi* ya Yehova yatasimama milele;^j
Mawazo ya moyo wake ni ya kizazi baada ya kizazi.
- 12 Lenye furaha ni taifa ambalo Mungu wake ni Yehova,^k
Watu ambao amewachagua kuwa miliki yake mwenyewe.^l
- 13 Yehova anatazama chini kutoka mbinguni;
Anawaona wanadamu wote.^m
- 14 Kutoka katika makao yake,

33:6 *Au "pumzi ya." #Au "jeshi lote la mbinguni liliumbwa." 33:8 *Au "ardhi inayozaa." 33:10 *Au "mashauri ya." #Au "mawazo." 33:11 *Au "mashauri."

SURA YA 33

a Ayu 37:23
Zb 11:7
Zb 45:7

b Zb 145:16
Mdo 14:17

c Ebr 11:3

d Mwa 1:9
Ayu 38:8-11
Met 8:29
Yer 5:22

e Ufu 14:7

f Zb 148:4, 5

g Zb 119:90

h Isa 8:10
Isa 19:3

i Zb 21:8, 11

j Met 19:21
Isa 46:10

k Kum 33:29

l Zb 65:4
Zb 135:4
1Pe 2:9

m Zb 11:4
Zb 14:2
Met 15:3
Ebr 4:13

Safu ya 2

a 1Nya 28:9
Ayu 34:21
Met 24:12

b Yos 11:6

c 2Nya 32:21
Zb 44:4, 5

d 2Fa 7:6, 7
Zb 20:7
Met 21:31
Isa 31:1

e Ayu 36:7
Zb 34:15

f Isa 33:15, 16

g Kum 33:29

h Zb 28:7
Met 18:10

i Zb 32:10

j Mik 7:7

SURA YA 34

k 1Sa 21:12, 13

- Anawakazia macho wakaaji wa dunia.
- 15 Yeye ndiye anayeumba mioyo ya wote;
Huchunguza kazi zao zote.^a
- 16 Hakuna mfalme anayeokolewa na jeshi kubwa;^b
Mtu hodari haokolewi na nguvu zake nyingi.^c
- 17 Farasi ni tumaini la uwongo la wokovu;^{#d}
Nguvu zake nyingi hazimhakikishii mtu kwamba ataponyoka.
- 18 Tazama! Jicho la Yehova linawalinda wale wanaomwogopa,^e
Wale wanaongojea upendo wake mshikamanifu,
- 19 Ili awaokoe* kutoka katika kifo
Na kuwahifadhi hai wakati wa njaa kali.^f
- 20 Tunamtarajia Yehova.
Yeye ni msaidizi wetu na ngao yetu.^g
- 21 Mioyo yetu hushangilia kwa sababu yake,
Kwa maana tunalitumaini jina lake takatifu.^h
- 22 Upendo wako mshikamanifu na ukae juu yetu,
Ee Yehova,ⁱ
Tunapoendelea kungojea.^j
- Wa Daudi, alipojifanya mwenda wazimu^k mbele ya Abimeleki, hivi kwamba akamfukuza, naye akaenda zake.
- ✠ [Aleph]
- 34 Nitamsifu Yehova nyakati zote;
Sifa yake itakuwa midomoni mwangu daima.

33:17 *Au "la ushindi." 33:19 *Au "aokoe nafsi zao."

⌒ [Beth]

2 Nitajigamba* kwa sababu ya Yehova;^a
Wapole watasikia na kushangilia.

⌒ [Gimel]

3 Mtukuzeni Yehova pamoja nami;^b
Na tulikweze jina lake pamoja.

⌒ [Daleth]

4 Nilimwomba Yehova ushauri, naye akanijibu.^c
Aliniokoa kutoka katika mambo yote yanayonio-gopesha.^d

⌒ [He]

5 Wale waliomtazama wali-ng'aa;
Nyuso zao hazingeweza kuona aibu.

⌒ [Zayin]

6 Mtu huyo wa hali ya chini aliita, na Yehova aka-sikia.
Alimwokoa kutoka katika taabu zake zote.^e

⌒ [Heth]

7 Malaika wa Yehova hupiga kambi pande zote kuwa-zunguka wanaomwogopa Yeye,^f
Naye huwaokoa.^g

⌒ [Teth]

8 Onjeni mwone kwamba Yehova ni mwema;^h
Mwenye furaha ni mtu anayemkimbilia.

⌒ [Yod]

9 Mwogopeni Yehova, ninyi nyote watakatifu wake,
Kwa maana wale wa-naomwogopa hawakosi chochote.ⁱ

⌒ [Kaph]

10 Hata wanasimba* wenye

SURA YA 34

a Yer 9:24
1Ko 1:31

b Zb 35:27

c Ebr 5:7

d Zb 18:48

e 2Sa 22:1

f 2Fa 6:17
Zb 91:11
Mt 18:10
Ebr 1:7, 14

g 2Fa 19:35
Da 6:22
Mdo 5:18, 19
Mdo 12:11

h 1Pe 2:3

i Zb 23:1
Flp 4:19

Safu ya 2

a Zb 23:6
Zb 84:11

b Ayu 28:28
Met 1:7
Met 8:13

c Kum 6:1, 2
Kum 30:19, 20
1Pe 3:10-12

d Yak 1:26
Yak 3:8

e Met 12:19
Met 15:4
1Pe 2:1

f Zb 37:27
Zb 97:10
Amo 5:15
Ro 12:9

g Mt 5:9
Ebr 12:14

h Ayu 36:7
Zb 33:18

i Zb 18:6
Isa 59:1

j Zb 37:10
Met 10:7

k Zb 145:18, 19

l 2Nya 32:22
Mdo 12:11

m Zb 147:3
Isa 61:1

n Zb 51:17
Isa 57:15
Isa 66:2

nguvu wamelemewa na njaa,
Lakini wale wanaomtafuta Yehova hawatakosa chochote chema.^a

⌒ [Lamed]

11 Njooni, wanangu, nisikilizeni;
Nitawafundisha kumwogopa Yehova.^b

⌒ [Mem]

12 Ni nani miongoni mwenu anayependa uzima Na angependa kuishi siku nyingi njema?^c

⌒ [Nun]

13 Basi ulinde ulimi wako usiseme mabaya,^d
Midomo yako isiseme uwongo.^e

⌒ [Samekh]

14 Acha uovu, utende mema;^f
Tafuta amani na uifuatie.^g

⌒ [Ayin]

15 Macho ya Yehova yanawatazama waadilifu,^h
Na masikio yake yanasiliza kilio chao cha kuomba msaada.ⁱ

⌒ [Pe]

16 Lakini uso wa Yehova uko dhidi ya wale wanaotenda maovu,
Ili afutilie mbali kumbukumbu lao lote kutoka duniani.^j

⌒ [Tsade]

17 Walilia kwa sauti, na Yehova akasikia;^k
Aliwaokoa kutoka katika taabu zao zote.^l

⌒ [Qoph]

18 Yehova yuko karibu na wale waliovunjika moyo,^m
Huwaokoa waliopondeka roho.^{*n}

34:2 *Au "Nafsi yangu itajigamba."

34:10 *Au "wanasimba wenye manyoya marefu shingoni ambao ni."

34:18 *Au "waliovunjika moyo."

⌌ [Resh]

- 19** Mwadilifu ana matatizo mengi,*^a
Lakini Yehova humwokoia kutoka katika matatizo hayo yote.^b
- ⌘ [Shin]
- 20** Anailinda mifupa yake yote;
Haujavunjwa hata mmoja.^c
- ⌌ [Taw]
- 21** Msiba utamuua mwovu;
Wale wanaomchukia mwadilifu watahesabiwa kuwa na hatia.
- 22** Yehova anaukomboa uhai wa* watumishi wake;
Hakuna yeyote anayemkimbililia atakayepatikana na hatia.^d

Wa Daudi.

- 35** Ee Yehova, itetee kesi yangu dhidi ya wapi-nzani wangu;^e
Pigana na wale wanaopigana nami.^f
- 2** Chukua ngao yako ndogo* na ngao yako kubwa,^g
Inuka unitetee.^h
- 3** Inua mkuki wako na shoka lako la vita* dhidi ya wale wanaonifuatia.ⁱ
Niambie: # “Mimi ni woko-vu wako.”^j
- 4** Wale wanaowinda uhai wangu* na waaibishwe na kufedhehesha.^k
Acha wale wanaopanga njama ya kuniangamiza wakimbie kwa aibu.
- 5** Na wawe kama makapi katika upepo;

34:19 *Au “misiba mingi.” 34:22 *Au “anaikomboa nafsi ya.” 35:2 *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale. 35:3 *Au “shoka lenye makali pande zote mbili.” #Au “lambie nafsi yangu.” 35:4 *Au “wanaowinda nafsi yangu.”

SURA YA 34

a Met 24:16
2Ti 3:12

b Da 6:21, 22
1Ko 10:13

c Yoh 19:36

d Zb 84:11

SURA YA 35

e 1Sa 24:15

f Zb 3:7

g Kut 15:3

h Isa 42:13

i 1Sa 23:26

j Isa 12:2

k Yer 17:18

Safu ya 2

a Kut 14:19, 20
Isa 37:36

b Zb 57:6
Zb 141:10

c Zb 18:17

d Zb 40:17
Met 22:22, 23

e Zb 27:12
Mt 26:59

f 1Sa 19:4, 5
1Sa 20:33
Yer 18:20

Malaika wa Yehova na awafukuze.^a

- 6** Njia yao na iwe na giza na utelezi
Malaika wa Yehova anapo-wafuatia.
- 7** Kwa maana bila sababu wameficha wavu wa kunitega;
Na bila sababu wamenichimbia shimo.
- 8** Msiba na umjie kwa ghafla;
Wavu aliouficha na umnase;
Na aanguke ndani yake na kuangamizwa.^b
- 9** Lakini mimi nitashangilia kwa sababu ya Yehova;
Nitakuwa na shangwe kwa sababu ya matendo yake ya wokovu.
- 10** Mifupa yangu yote itasema:
“Ee Yehova, ni nani aliye kama wewe?
Unawaokoa wasio na uwezo kutoka kwa wale wanaowazidi nguvu,^c
Wasio na uwezo na maskini kutoka kwa wale wanaowanyang’anya.”^d
- 11** Mashahidi wenye nia mba-ya hunikabili,^e
Na kuniuliza mambo nisi-yoyajua.
- 12** Wananilipa uovu kwa mema niliyotenda,^f
Na kunifanya nihisi kama mtu aliyefiwa.
- 13** Lakini walipokuwa wago-njwa, nilivaa nguo za magunia;
Nilijitesa kwa kufunga,
Na sala yangu ilipokosa kujibiwa,*

35:13 *Au “iliporudi kwenye kifua changu.”

- 14** Nilitembea huku na huku nikiomboleza kana kwa-mba ninamwombolezea rafiki au ndugu yangu; Niliinama chini kwa huzuni, kama mtu anayemwombolezea mama yake.
- 15** Lakini nilipojikwaa, walishangilia na kuku-sanyika pamoja; Walikusanyika pamoja ili wanivizie na kuniua; Walinirarua vipandevipande nao hawakunyamaza.
- 16** Wasiomwogopa Mungu wanandihaki kwa dhauru,* Wananisagia meno yao.^a
- 17** Ee Yehova, utatazama tu mpaka lini?^b Niokoe dhidi ya masha-mbulizi yao,^c Uhai wangu wenye thamani* kutoka kwa wanasimba.^d
- 18** Kisha nitakushukuru katika kutaniko kubwa;^e Nitakusifu katikati ya umati wa watu.
- 19** Usiruhusu wale ambao ni maadui wangu bila saba-bu wanicheke; Usiruhusu wale wanao-nichukia bila sababu^f wakonyeze macho yao kwa hila.^g
- 20** Kwa maana hawasemi maneno ya amani, Lakini wanapanga njama kwa hila dhidi ya watu wenye amani nchini.^h

35:16 *Au labda, "Wasiomwogopa Mungu wanadhihaki ili wapate keki."
35:17 *Tnn., "Uhai pekee nilio nao," yaani, nafsi yake. ^aAu "wanasimba wenye manyoya marefu shingoni."

SURA YA 35

a Zb 37:12

b Hab 1:13

c Zb 142:6

d Zb 22:20
Zb 57:4

e Zb 22:22

f Zb 69:4
Yoh 15:24, 25

g Met 6:12, 13

h Zb 31:13
Yer 11:19
Mt 26:4

Safu ya 2

a Zb 28:1

b Zb 10:1
Zb 71:12c Zb 26:1
Zb 96:13

d Zb 41:1, 2

e Zb 84:11
Zb 149:4

f Zb 51:14

g Zb 71:24

SURA YA 36

h Ro 3:18

- 21** Wanafungua kinywa chao wazi ili wanishtaki, Wakisema: "Aha! Aha! Macho yetu yameliona."
- 22** Ee Yehova, umeona jambo hilo. Usinyamaze.^a Ee Yehova, usikae mbali nami.^b
- 23** Amka, inuka unitetee, Mungu wangu, Yehova, nitetee katika kesi yangu.
- 24** Nihukumu kulingana na uadilifu wako,^c Ee Yehova Mungu wangu; Usiruhusu wanicheke.
- 25** Wasiseme kamwe moyoni mwao: "Aha! Tulipata tulichotaka!"* Wasiseme kamwe: "Tume-mmeza."^d
- 26** Acha wote waaibishwe na kufedheheshwa, Wale wanaonicheka kwa sababu ya msiba wangu. Acha wale wanaojikweza juu yangu wavishwe aibu na fedheha.
- 27** Lakini acha wale wanao-furahia uadilifu wangu wapaze sauti kwa shangwe; Na waseme daima: "Yehova na atukuzwe, anayefurahia amani ya mtumishi wake."^e
- 28** Kisha ulimi wangu utasimulia* uadilifu wako^f Na kukusifu mchana kutwa.^g Kwa kiongozi. Wa Daudi, mtumishi wa Yehova.
- 36** Dhambi huzungumza na mwovu ndani kabisa ya moyo wake; Hakuna hofu ya Mungu mbele ya macho yake.^h

35:25 *Au "Aha! Nafsi yetu." **35:28** *Au "utatafakari."

- 2** Kwa maana hujisifusifu sana machoni pake mwenyewe
Hivi kwamba hawezi kutambua kosa lake na kulichukia.^a
- 3** Maneno ya kinywa chake yanadhuru na ni ya udanganyifu;
Haonyeshi ufahamu wowote wa kutenda mema.
- 4** Hupanga njama zinazodhuru hata kitandani mwake.
Hufuatia njia isiyo njema; Hakatai lililo baya.
- 5** Ee Yehova, upendo wako mshikamanifu unafika mpaka mbinguni,^b
Uaminifu wako mpaka mawinguni.
- 6** Uadilifu wako ni kama milima mikubwa;^{*c}
Hukumu zako ni kama maji mengi yenye kina.^d
Unawahifadhi* wanadamu na wanyama, Ee Yehova.^e
- 7** Jinsi upendo wako mshikamanifu ulivyo na thamani sana, Ee Mungu!^f
Katika kivuli cha mabawa yako, wanadamu hukimbilia.^g
- 8** Wanakunywa na kushiba vitu vinono vya* nyumba yako,^h
Nawe huwanywesha kwenye kijito cha vitu vyako vinavyofurahisha.ⁱ
- 9** Wewe ndiye chanzo cha uhai;^j
Kwa nuru yako tunaweza kuona nuru.^k

36:6 *Tnn., "kama milima ya Mungu."
#Au "Unawaokoa." 36:8 *Tnn., "mafuta ya."

SURA YA 36

a Kum 29:19, 20

b Zb 103:11

c Zb 71:19

d Ro 11:33

e Zb 145:9
1Ti 4:10

f Mik 7:18

g Ru 2:12
Zb 17:8
Zb 91:4

h Zb 65:4

i Zb 16:11

j Ayu 33:4
Yer 2:13
Mdo 17:28
Ufu 4:11k Zb 27:1
Zb 43:3
Yak 1:17
1Pe 2:9

Safu ya 2

a Zb 103:17

b Zb 7:10
Zb 97:11

c Zb 1:5

SURA YA 37

d Zb 73:3
Met 23:17

e Zb 73:12, 19

f Isa 1:17
Ebr 13:16

g Met 28:20

h Zb 55:22
Met 16:3i Mt 6:33
Flp 4:6
1Pe 5:6, 7

- 10** Endelea kuwatendea kwa upendo wako mshikamanifu wale wanaokujua,^a
Na kuwaonyesha uadilifu wako walio wanyoofu moyoni.^b

- 11** Usiruhusu mguu wa mwenye kiburi unikanyage
Wala mkono wa mwovu unifikuze.

- 12** Watenda maovu wameanguka huko;
Wamepigwa na kuangu-shwa chini na hawawezi kusimama.^c

Wa Daudi.

N [Aleph]

- 37** Usikasirike* kwa sababu ya waovu
Wala usiwaonee wivu watenda dhambi.^d

- 2** Watanyauka haraka kama majani^e
Na kusinyaa kama majani yaliyochipuka ya kijani kibichi.

M [Beth]

- 3** Mtumaini Yehova na utende mema;^f
Kaa duniani,* na utende kwa uaminifu.^g
- 4** Pata furaha tele* katika Yehova,
Naye atatosheleza tamaa za moyo wako.

N [Gime]

- 5** Mkabidhi* Yehova njia yako;^h
Mtegemee yeye, naye atenda kwa niaba yako.ⁱ
- 6** Ataufanya uadilifu wako ung'ae kama mapambazuko,
Na haki yako kama jua la adhuhuri.

37:1 *Au "Usiwake hasira." 37:3 *Au "nchini." 37:4 *Au "Pata shangwe nyingi sana." 37:5 *Tnn., "Mvingirishie."

𐤀 [Daleth]

- 7 Nyamaza mbele za
Yehova^a
Na umngojee kwa matu-
maini.*
Usikasirishiwa na mtu
Anayefanikiwa kutekeleza
njama zake.^b

𐤀 [He]

- 8 Acha hasira na uache
ghadhabu;^c
Usikasirike na kuanza
kutenda uovu.*
9 Kwa maana waovu wataa-
ngamizwa,^d
Lakini wale wanaomtumai-
ni Yehova wataimiliki
dunia.^e

𐤀 [Waw]

- 10 Bado muda mfupi tu, na
watu waovu hawataku-
wepo tena;^f
Utapaangalia mahali wali-
pokuwa,
Nao hawatakuwepo.^g
11 Lakini wapole wataimiliki
dunia,^h
Nao watafurahia kweli-
kweli wingi wa amani.ⁱ

𐤀 [Zayin]

- 12 Mtu mwovu hupanga nja-
ma dhidi ya mwadilifu;^j
Humsagia meno yake.
13 Lakini Yehova atamcheka,
Kwa maana Anajua kwa-
mba siku yake itakuja.^k

𐤀 [Heth]

- 14 Waovu huchomoa panga
zao na kuzikunja* pinde
zao
Ili kumwangusha chini ali-
yekandamizwa na pia
maskini,

37:7 *Au "subira." 37:8 *Au labda,
"Usikasirike, kwa maana hasira itakuo-
ngoza tu kwenye madhara." 37:14 *Au
"kuzitia nyuzi."

SURA YA 37

a Zb 62:1
Omb 3:26

b Ayu 21:7
Zb 73:3
Yer 12:1

c Met 14:29
Efe 4:26

d Zb 55:23

e Zb 25:12, 13
Zb 37:29
Mt 5:5
2Pe 2:9

f Ayu 24:24

g 1Sa 25:39
Zb 52:4, 5

h Isa 45:18
Mt 5:5
Ufu 21:3

i Zb 72:7
Zb 119:165
Isa 48:18

j 1Sa 18:21, 25

k 1Sa 26:9, 10

Safu ya 2

a 2Sa 17:23
Est 7:10
Zb 7:15

b Met 16:8
Met 30:8, 9
1Ti 6:6

c Zb 16:11

d Met 10:7

e Kum 15:11
Ayu 31:16, 22
Zb 112:9
Met 19:17

f Zb 37:9

g Met 16:9

Ili kuwachinja wale ambao
njia yao imenyooka.

- 15 Lakini upanga wao utau-
choma moyo wao
wenyewe;^a
Pinde zao zitavunjwa.

𐤀 [Teth]

- 16 Kidogo alichu nacho
mwadilifu ni bora
Kuliko wingi wa vitu
walivyo navyo watu
wengi waovu.^b
17 Kwa maana mikono ya
waovu itavunjwa,
Lakini Yehova atawatege-
meza waadilifu.

𐤀 [Yod]

- 18 Yehova anajua mambo
wanayokabili watu wasio
na lawama,*
Na urithi wao utadumu
milele.^c
19 Hawataaibishwa wakati
wa msiba;
Wakati wa njaa kali wata-
kuwa na chakula tele.

𐤀 [Kaph]

- 20 Lakini waovu wataanga-
mia;^d
Maudu wa Yehova watato-
weka kama malisho bora
kabisa;
Watatoweka kama moshi.

𐤀 [Lamed]

- 21 Mwovu hukopa lakini
halipi,
Lakini mwadilifu ni mkari-
mu* naye hutoa.^e
22 Wale Anaowabariki watai-
miliki dunia,
Lakini wale Anaowalaani
wataangamizwa.^f

𐤀 [Mem]

- 23 Yehova huongoza* hatua
za mtu^g

37:18 *Tnn., "siku za wasio na lawama."
37:21 *Au "hufadhili." 37:23 *Au "hui-
marisha."

Njia ya mtu huyo inapompendeza Yeye.^a

- 24 Hata akianguka, hataangukwa chini kabisa,^b
Kwa maana Yehova anau-shika mkono wake na kumtegemeza.*^c

‡ [Num]

- 25 Nilikuwa kijana lakini sasa nimezeeka,
Lakini sijamwona mtu yeyote mwadilifu akiwa ameachwa,^d
Wala watoto wake wakita-futa mkate.*^e

- 26 Sikuzote anakopesha bila faida,^f
Na watoto wake watapata baraka.

‡ [Samekh]

- 27 Acha uovu, utende mema,^g
Nawe utaishi milele.

- 28 Kwa maana Yehova anapenda haki,
Naye hatawaacha washikamanifu wake.^h

‡ [Ayin]

Watalindwa sikuzote;ⁱ
Lakini wazao wa waovu wataangamizwa.^j

- 29 Waadilifu wataimiliki dunia,^k
Nao wataishi humo milele.^l

‡ [Pe]

- 30 Kinywa cha mwadilifu hufundisha hekima,*
Na ulimi wake huongea kuhusu haki.^m

- 31 Sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake;ⁿ
Hatua zake hazitayumba-umba.^o

37:24 *Au "anamtegemeza kwa mkono Wake." 37:25 *Au "chakula." 37:30 *Au "huzungumza hekima kwa sauti ya chini."

SURA YA 37

a Met 11:20

b Zb 34:19
Met 24:16

c Zb 91:11, 12

d Zb 94:14
Mt 6:33
Ebr 13:5

e Kum 24:19
Zb 145:15
Met 10:3

f Kum 15:7, 8
Zb 112:5

g Zb 34:14
Isa 1:17

h 2Sa 22:26

i Zb 97:10
Met 2:7, 8

j Met 2:22

k Kum 30:20
Zb 37:9
Met 2:21
Mt 5:5

l Mt 25:46
Ufu 21:3, 4

m Mt 12:35
Efe 4:29
Kol 4:6

n Kum 6:6
Zb 40:8

o Zb 121:3

Safu ya 2

a 2Pe 2:9

b Zb 109:31

c Zb 37:22

d Zb 52:5, 6

e Est 5:11
Ayu 21:7

f Kut 15:9, 10

g Zb 37:10

h Ayu 1:1

i Ayu 42:12, 16

j Zb 1:4
Met 10:7
2Pe 2:9

k Isa 12:2

l Zb 9:9
Isa 33:2

m Isa 46:4
1Ko 10:13

‡ [Tsade]

- 32 Mwovu humtazama mwadilifu,
Akitafuta kumuua.

- 33 Lakini Yehova hatamwacha mikononi mwa mtu huyo^a
Wala hatampata na hatia anapohukumiwa.^b

‡ [Qoph]

- 34 Mtumaini Yehova na ufuate njia yake,
Naye atakukweza uimiliki dunia.
Waovu watakapoangami-zwa,^c utaona jambo hilo.^d

‡ [Resh]

- 35 Nimemwona mtu mkatili, mwovu
Akisambaa kama mti wenyewe majani mengi katika udongo wake wa asili.^e

- 36 Lakini alikufa ghafla naye akatoweka;^f
Niliendelea kumtafuta, lakini sikuweza kumpata.^g

‡ [Sin]

- 37 Mwangalie mtu asiye na lawama,*
Na uendelee kumwangelia mnyoofu,^h
Kwa maana wakati ujao wa mtu huyo utakuwa na amani.ⁱ

- 38 Lakini watenda dhambi wote wataangamizwa;
Wakati ujao wa watu waovu utakomeshwa.^j

‡ [Taw]

- 39 Wokovu wa watu waadilifu unatoka kwa Yehova;^k
Yeye ndiye ngome yao wakati wa taabu.^l

- 40 Yehova atawasaidia na kuwaokoa.^m

37:37 *Au "mtu anayeshika utimilifu."

Atawanusuru kutoka kwa waovu na kuwaokoa, Kwa sababu wanamkimbi-lia yeye.^a

Muziki wa Daudi, wa kukumbusha.

- 38** Ee Yehova, usinikaripie kwa hasira yako, Wala usinirekebishe kwa ghadhabu yako.^b
- 2** Kwa maana mishale yako imenichoma ndani kabisa, Na mkono wako unanikandamiza chini.^c
- 3** Mwili wangu wote ni mgonjwa kwa sababu ya hasira yako kali. Hakuna amani katika mifupa yangu kwa sababu ya dhambi yangu.^d
- 4** Kwa maana dhambi zangu zimetanda juu ya kichwa changu;^e Kama mzigo mzito, ni nzi-to sana siwezi kuzibeba.
- 5** Vidonda vyangu vinanuka na vina usaha Kwa sababu ya upumbavu wangu.
- 6** Nimesononeka na kushuka moyo kupita kiasi; Ninatembea huku na huku mchana kutwa kwa huzuni.
- 7** Ninaungua ndani ya mwili wangu;* Mwili wangu wote ni mgonjwa.^f
- 8** Nimekufa ganzi na kupondeka kabisa; Moyo wangu wenye maumivu makali unanifanya nilie kwa sauti kubwa.*
- 9** Ee Yehova, unajua mambo yote ninayotamani,

38:7 *Tnn., "Viuno vyangu vimejaa moto." 38:8 *Au "ningurume."

SURA YA 37

a Zb 22:4
Da 3:17
Da 6:23

SURA YA 38

b Yer 10:24

c Zb 32:4

d Zb 6:2
Zb 41:4
Zb 51:8

e Ezr 9:6
Zb 40:12

f Zb 38:3

Safu ya 2

a Zb 6:7

b 2Sa 16:7
Zb 62:4

c 2Sa 16:11

d Zb 39:2, 9

e 2Sa 16:12
Zb 123:2

f Zb 138:3

g Zb 77:2

h Zb 32:5

i Zb 51:3

Na kilio changu cha maumivu hakijafichwa machoni pako.

- 10** Moyo wangu unadundunda, nguvu zangu zimetoweka, Na nuru ya macho yangu imetoweka.^a
- 11** Rafiki zangu na wenzangu wananiepuka kwa sababu ya pigo langu, Na rafiki zangu wa karibu wanasimama mbali.
- 12** Wale wanaotafuta uhai wangu* wanatega mitego; Wale wanaojaribu kuni-dhuru wanazungumza kuhusu kuniangamiza;^b Wananong'onezana uwongo mchana kutwa.
- 13** Lakini kama kiziwi, sikuwasikiliza;^c Na kama bubu, sikufumbua kinywa changu.^d
- 14** Nimekuwa kama mtu asiye-weza kusikia, Ambaye kinywa chake hakina lolote la kujitetea.
- 15** Kwa maana nilikungojea wewe, Ee Yehova,^e Nawe ukanjibu, Ee Yehova Mungu wangu.^f
- 16** Kwa maana nilisema: "Acha wasinicheke Wala kujikweza juu yangu mguu wangu ukiteleza."
- 17** Kwa maana nilikuwa kari-bu kuanguka, Na maumivu yangu yalikuwa pamoja nami daima.^g
- 18** Niliungama kosa langu;^h Nilihangaishwa na dhambi yangu.ⁱ

38:12 *Au "nafsi yangu."

- 19** Lakini maadui wangu wana juhudi* na ni hodari,[#]
Wale wanaonichukia bila sababu wameongezeka sana.
- 20** Walinilipa uovu kwa mema niliyotenda;
Walinipinga kwa sababu ya kufuatia mambo mema.
- 21** Usiniache, Ee Yehova.
Ee Mungu, usiendeleo kukaa mbali nami.^a
- 22** Njoo haraka unisaidie, Ee Yehova, wokovu wangu.^b
- Kwa kiongozi; wa Yeduthuni.^{*c}
Muziki wa Daudi.
- 39** Nilisema: “Nitailinda hatua yangu
Ili niepuke kutenda dhambi kwa ulimi wangu.^d
Nitakilinda kinywa changu kwa lijamu^e
Maadamu mtu yeyote mwovu yuko mbele yangu.”
- 2** Nilinyamaza na kukaa kima;^f
Niliendelea kunyamaza hata kuhusu jambo jema, Lakini maumivu yangu yalikuwa makali.*
- 3** Moyo wangu uliteketea polepole* ndani yangu. Nilipokuwa nikiwaza sana,[#] moto huo uliendelea kuwaka.
Kisha ulimi wangu uka-sema:
- 4** “Ee Yehova, nisaidie kujua mwisho wangu,

38:19 *Tnn., “wako hai.” [#]Au labda, “Lakini wale ambao ni maadui wangu bila sababu ni wengi.” **39:Uta** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **39:2** *Au “yalichochea.” **39:3** *Tnn., “uliwaka moto.” [#]Au “nikipiga kite.”

SURA YA 38

a Zb 22:11
Zb 35:22

b Zb 27:1
Zb 62:2
Isa 12:2

SURA YA 39

c 1Nya 16:41
1Nya 25:1

d Met 18:21

e Zb 141:3

f Zb 38:13
Mt 27:12
1Pe 2:23

Safu ya 2

a Zb 90:12

b Zb 90:9
Yak 4:14

c Zb 90:4

d Zb 62:9
Zb 144:4

e Zb 49:10
Mhu 2:18, 19
Mhu 4:8
Lu 12:19, 20

f Zb 25:11
Mik 7:19

g Ayu 40:4
Zb 38:13

h 2Sa 16:10

i Zb 90:8

Na idadi ya siku zangu,^a
Ili nijue ufupi wa maisha yangu.*

- 5** Kwa kweli, umefanya siku zangu ziwe chache tu;^{*b}
Na urefu wa maisha yangu kuwa si kitu mbele zako.^c

Kwa hakika kila mwanadamu, ingawa anaonekana yuko salama, si kitu ila pumzi tu.^d (*Sela*)

- 6** Kwa hakika kila mwanadamu hutembea huku na huku kama kivuli.
Hukimbia huku na huku* bila sababu.

Hurundika mali, bila kujua ni nani atakayeifurahia.^e

- 7** Sasa basi, ninaweza kutumaini nini, Ee Yehova?
Wewe ndiye tumaini langu pekee.

- 8** Niokoe kutoka katika makosa yangu yote.^f
Usimruhusu mpumbavu anifanye kuwa kitu cha kudharauliwa.

- 9** Niliendelea kunyamaza; Sikuweza kufumbua kinywa changu,^g
Kwa maana wewe ndiye uliyefanya hayo.^h

- 10** Niondolee pigo lako.
Nimedhoofika kabisa kwa sababu mkono wako unanipiga.

- 11** Unamrekebishwa mwanadamu kwa kumwadhibu kwa sababu ya kosa lake;ⁱ
Unaharibu kabisa vitu anavyothamini sana kama nondo* anavyoharibu.

39:4 *Au “nijue jinsi ninavyopita upesi.”
39:5 *Tnn., “ziwe vipimo vya mkono.”
39:6 *Tnn., “Hupiga kelele.” **39:11** *Aina fulani ya wadudu waharibifu.

Kwa kweli kila mwanadamu ni pumzi tu.^a (*Sela*)

- 12** Sikia sala yangu, Ee Yehova,
Sikiliza kilio changu cha kuomba msaada.^b
Usipuuzе machozi yangu.
Kwa maana kwako, mimi ni mkaaji mgeni tu,^c
Msafiri apitaye, * kama mababu zangu wote.^d
- 13** Usinitazame kwa ukali ili nichangamke
Kabla sijafa * na kuto-weka.”

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

- 40** Nilimtumaini Yehova kwa bidii, *
Naye akanitegea sikio lake na kusikia[#] kilio changu cha kuomba msaada.^e
- 2** Akanipandisha kutoka katika shimo linalonguruma,
Kutoka katika matope yenye utelezi.
Akaiweka miguu yangu juu ya jabali;
Akanifanya nisimame mahali palipo imara.
- 3** Kisha akaweka wimbo mpya kinywani mwangu,^f
Asifiwe Mungu wetu.
Wengi watatazama kwa hofu
Na kumtumaini Yehova.
- 4** Mwenye furaha ni mtu anayemtumaini Yehova
Na ambaye hawatumaini wakaidi au watu wadanganifyu. *

39:12 *Au “Mlowezi.” 39:13 *Tnn., “sijapita.” 40:1 *Au “Nilimngojea Yehova kwa subira.” #Au “akainama chini ili kunisikiliza, akasikia.” 40:4 *Au “wango.”

SURA YA 39

a Zb 39:5
Zb 102:11

b Zb 28:1

c Law 25:23
1Nya 29:15

d Ebr 11:13

SURA YA 40

e Zb 34:15

f Zb 33:3
Zb 98:1

Safu ya 2

a Ufu 15:3

b Kut 15:11

c Zb 139:17, 18

d 1Sa 15:22
Zb 51:16, 17
Ho 6:6

e Isa 50:5

f Ebr 10:5-9

g Lu 24:44

h Yoh 4:34

i Zb 37:31
Ro 7:22

j Zb 22:22

k Ebr 13:15

l Ebr 2:12

- 5** Jinsi ulivyotenda mambo mengi sana,
Ee Yehova Mungu wangu,
Kazi zako zinazostaajabisha na mawazo yako kutuelekea.^a
Hakuna yeyote anayeweza kulinganishwa nawe;^b
Ikiwa ningejaribu kusimulia na kuongea kuzihusu, Zingekuwa nyingi sana kwangu kusimulia!^c
- 6** Hukutamani * dhabihu na toleo,^d
Lakini ulifungua masikio yangu ili yasikie.^e
Hukuomba dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za dhambi.^f
- 7** Kisha nikasema: “Tazama, nimekuja.
Katika kitabu cha kunjwa imeandikwa kunihusu.^g
- 8** Ee Mungu wangu, ninafuraha * kufanya mapenzi yako,^h
Na sheria yako imo ndani yangu kabisa.ⁱ
- 9** Ninatangaza habari njema ya uadilifu katika kutaniko kubwa.^j
Tazama! Siizui midomo yangu,^k
Ee Yehova, kama unavyojua vema.
- 10** Siufuniki uadilifu wako moyoni mwangu.
Ninatangaza uaminifu wako na wokovu wako.
Siufichi upendo wako mshikamanifu na ukweli wako katika kutaniko kubwa.”^l
- 11** Ee Yehova, usininyime rehema yako.

40:6 *Au “Hukupendezwa na.” 40:8 *Au “ninatamani.”

Upendo wako mshikamafu na ukweli wako na unilinde daima.^a

- 12** Misiba inayonizunguka ni mingi sana haihesabiki.^b

Makosa yangu mengi yananilemea hivi kwamba siwezi kuona njia yangu;^c
Ni mengi sana kuliko nywele za kichwa changu,
Nami nimevunjika moyo.

- 13** Tafadhali, Ee Yehova, uwe tayari kuniokoa.^d
Ee Yehova, njoo haraka unisaidie.^e

- 14** Wote wanaotaka kuniua* Na waaibishwe na kufedhehesha.
Wale wanaofurahia msiba wangu
Na wakimbie kwa aibu.

- 15** Wale wanaoniambia: "Aha! Aha!"
Na washtuke kwa sababu ya aibu yao.

- 16** Lakini acha wale wanaokutafuta^f
Wafurahi na kushangilia kwa sababu yako.^g
Wale wanaopenda matendo yako ya wokovu na waseme daima:

"Yehova na atukuzwe."^h

- 17** Lakini sina uwezo, nami ni maskini;
Yehova na anitunze.
Wewe ni msaidizi wangu na mwokozi wangu;ⁱ
Mungu wangu, usikawie.^j

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

- 41** Mwenye furaha ni mtu yeyote anayemjali mtu wa hali ya chini;^k
Yehova atamwokoza siku ya msiba.

40:14 *Au "wanaoitafuta nafsi yangu."

SURA YA 40

a Zb 61:6, 7

b Zb 71:20

c Zb 38:4

d Zb 25:17

e Zb 38:22
Zb 70:1-5

f Kum 4:29

g Zb 13:5

h Zb 35:27

i Zb 54:4
Isa 50:7
Ebr 13:6

j Zb 143:7

SURA YA 41

k Kum 15:7, 8
Zb 112:9
Met 14:21
Met 22:9

Safu ya 2

a Mt 5:7

b 2Pe 2:9

c 2Fa 20:5
Zb 103:3

d Zb 51:1

e Zb 6:2
Zb 147:3

f Zb 32:5
Zb 38:3
Met 28:13

g Zb 3:2
Zb 71:10, 11

h 2Sa 15:12
Ayu 19:19
Zb 55:12, 13

- 2** Yehova atamlinda na kumhifadhi hai.
Atatangazwa kuwa mwenye furaha duniani;^a
Hutamtia kamwe mikononi mwa maadui wake ili wamtendee wape ndavyo.^{*b}

- 3** Yehova atamtegemeza kwenye kitanda chake cha ugonjwa;^c
Wakati huo wa ugonjwa utakibadili kabisa kitanda chake.

- 4** Kwa maana nilisema: "Ee Yehova, nionyeshe kibali."^d
Niponye,^{*e} kwa maana nimekutendea dhambi."^f

- 5** Lakini maadui wangu wanasema mambo maovu kunihusu:
"Atakufa lini jina lake lito weke?"

- 6** Mmoja wao akija kuniona, moyo wake husema uwongo.
Hukusanya mambo yenye kudhuru ya kusema;
Kisha hutoka nje na kuyae neza kotekote.

- 7** Wote wanaonichukia wananong'onezana;
Wanapanga njama ya uovu dhidi yangu:

- 8** "Amepatwa na jambo linaloogopesha;
Sasa kwa kuwa yuko chini, hatainuka tena."^g

- 9** Hata mtu niliyekuwa na amani naye, ambaye nilimwamini,^h

41:2 *Au "Hutamtia kamwe katika tamaa ya maadui wake; au katika nafsi ya maadui wake." Angalia Kamusi, uku. 2012. 41:4 *Au "Iponye nafsi yangu."

Aliyekuwa akila mkate wangu, amekiinua kisigino chake dhidi yangu.*^a

- 10** Lakini wewe, Ee Yehova, nionyeshe kibali na kuiniinua,
Ili niwalipize.
- 11** Kwa njia hii nitajua kwa mba unapendezwa nami: Adui yangu asipoweza ku-

41:9 *Au "amenigeuka."

SURA YA 41

a Mk 14:18
Yoh 13:18
Yoh 13:26

Safu ya 2

a Zb 31:8
Yer 20:13

b Zb 25:21
Met 2:7

c Zb 34:15

d 1Nya 16:36
1Nya 29:10

paza sauti kwa ushindi dhidi yangu.^a

- 12** Lakini mimi, unanitegemeza kwa sababu ya utimilifu wangu;^b Utaniweka mbele zako* milele.^c
- 13** Yehova, Mungu wa Israeli, na asifiwe
Kwa umilele wote.*^d
Amina na Amina.

41:12 *Tnn., "mbele za uwepo wako."

41:13 *Au "Milele na milele."

KITABU CHA PILI
(Zaburi 42-72)

Kwa kiongozi.
Maskili* ya wana wa Kora.^a

- 42** Kama paa anayetamani vijito vya maji,
Ndivyo ninavyokutamani,
Ee Mungu.

- 2** Nina kiu kwa ajili ya Mungu, kwa ajili ya Mungu aliye hai.^b
Nije lini na kuonekana mbele za Mungu?^c

- 3** Machozi yangu ni chakula changu usiku na mchana;
Mchana kutwa watu wanandihaki wakisema:
"Mungu wako yuko wapi?"^d

- 4** Ninayakumbuka mambo haya, nami naimwaga nafsi* yangu,
Kwa maana wakati fulani nilitembea pamoja na umati;
Nilikuwa nikitembea kiyakimya[#] mbele zao kwenda katika nyumba ya Mungu,
Kwa sauti za shangwe na shukrani,

42:Uta; 42:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012. **42:4** [#]Au "polepole."

SURA YA 42

a 2Nya 20:19

b Zb 63:1

c Zb 27:4
Zb 84:2

d Zb 3:2
Zb 42:10
Zb 79:10

Safu ya 2

a Kum 16:14, 16
2Nya 30:23, 24

b Zb 55:4
Mk 14:34

c Zb 37:7
Omb 3:24
Mik 7:7

d Zb 43:5

e Zb 22:1
Yoh 12:27

f Yon 2:7

g Zb 88:7

Za umati unaofanya sherehe.^a

- 5** Kwa nini nimesononeka?^b
Kwa nini msukosuko huu umo ndani yangu?

Mngojee Mungu,^c
Kwa maana bado nitamsifu kwa kuwa yeye ni Mwokozi wangu Mtu-kufu.^d

- 6** Mungu wangu, nimesononeka.^e
Ndiyo sababu ninakukumbuka,^f

Kutoka katika nchi ya Yordani na vilele vya Hermoni,

Kutoka Mlima Mizari.*

- 7** Vilindi vya maji vinaita vilindi vya maji
Kwa sauti ya maporomoko yako ya maji.

Mawimbi yako makubwa yamenilemea.^g

- 8** Wakati wa mchana Yehova atanipa upendo wake mshikamanifu,
Na usiku wimbo wake utakuwa pamoja nami—sala

42:6 *Au "ule mlima mdogo."

kwa Mungu wa uhai wangu.^a

- 9 Nitamwambia Mungu, jabali langu:

“Kwa nini umenisahau?^b

Kwa nini nitembe huku na huku nikiwa na huzuni kwa sababu ya kukandamizwa na adui yangu?”^c

- 10 Maadui wangu wananidhahi kwa chuki kali sana; **

Mchana kutwa wananidhahi wakisema: “Mungu wako yuko wapi?”^d

- 11 Kwa nini nimesononeka? Kwa nini msukosuko huu umo ndani yangu?

Mngojee Mungu,^e

Kwa maana bado nitamsifu kwa kuwa yeye ni Mwokozi wangu Mtukufu na Mungu wangu.^f

- 43 Nihukumu, Ee Mungu,^g Itete kesi yangu^h dhidi ya taifa lisilo na ushi-kamanifu.

Niokoe kutoka kwa mtu mdanganyifu na asiye mwadilifu.

- 2 Kwa maana wewe ni Mungu wangu, ngome yangu.ⁱ

Kwa nini umenitupa?

Kwa nini nitembe huku na huku nikiwa na huzuni kwa sababu ya kukandamizwa na adui yangu?^j

- 3 Itume nuru yako na kweli yako.^k

Navyo viniongoze;^l

Viniongoze kwenye mlima

42:10 *Yaani, inayoweza kusababisha mauaji. ^a Au labda, “kana kwamba wanaiponda mifupa yangu.”

SURA YA 42

a Zb 27:1

b Zb 13:1

c Zb 38:6
Zb 43:2

d Zb 3:2
Zb 42:3
Zb 79:10

e Zb 37:7

f Zb 42:5
Zb 43:5

SURA YA 43

g Zb 26:1
Zb 35:24

h Zb 35:1
Met 22:22, 23

i Zb 28:7
Zb 140:7

j Zb 42:9

k Zb 40:11
Met 6:23

l Zb 5:8
Zb 27:11
Zb 143:10

Safu ya 2

a 1Nya 16:1
Zb 78:68, 69

b Zb 84:3

c 2Sa 6:5

d Zb 37:7

e Zb 42:5, 11

SURA YA 44

f 2Nya 20:19

g Kut 13:14
Hes 21:14
Amu 6:13

h Kum 7:1

i Kut 15:17
Zb 78:55
Zb 80:8, 9

j Yos 10:5, 11
Zb 135:10, 11

k Kum 4:38
Yos 24:12

l 1Sa 12:22

m Isa 63:11-13

n Kum 7:7, 8

o Zb 74:12
Isa 33:22

wako mtakatifu na kwenye hema lako tukufu la ibada.^a

- 4 Kisha nitakuja kwenye madhabahu ya Mungu,^b

Kwa Mungu, shangwe yangu inayofurika.

Nami nitakusifu kwa kinubi,^c Ee Mungu, Mungu wangu.

- 5 Kwa nini nimesononeka?

Kwa nini msukosuko huu umo ndani yangu?

Mngojee Mungu,^d

Kwa maana bado nitamsifu kwa kuwa yeye ni Mwokozi wangu Mtukufu na Mungu wangu.^e

Kwa kiongozi.

Wa wana wa Kora.^f Maskili. *

- 44 Ee Mungu, tumesikia kwa masikio yetu wenyewe,

Mababu zetu wametusi-mulia,^g

Mambo uliyotimiza katika siku zao,

Siku za zamani za kale.

- 2 Kwa mkono wako uliyafukuza mataifa^h

Ukawafanya mababu zetu waishi huko.ⁱ

Uliyapondaponda mataifa na kuyafukuza.^j

- 3 Hawakuimiliki nchi kwa upanga wao wenyewe,^k

Na mkono wao wenyewe haukuwaletea ushindi.^l

Badala yake, waliimiliki kwa mkono wako wa

kuume na uwezo wako^m na nuru ya uso wako,

Kwa maana ulipendezwa nao.ⁿ

- 4 Wewe ni Mfalme wangu, Ee Mungu;^o

44:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.

- Amuru* ushindi kamili#
kwa ajili ya Yakobo.
- 5 Kwa nguvu zako tutawafu-
kuza maadui wetu;^a
Katika jina lako tutawa-
kanyagia chini wale
wanaoinuka dhidi yetu.^b
- 6 Kwa maana siutumaini
upinde wangu,
Na upanga wangu hauwezi
kuniokoa.^c
- 7 Ni wewe uliyetuokoa kuto-
ka kwa maadui wetu,^d
Wewe uliyewaaibisha wale
wanaotuchukia.
- 8 Tutamsifu Mungu mchana
kutwa,
Nasi tatalishukuru jina
lako milele. (*Sela*)
- 9 Lakini sasa umetutupa na
kutuaibisha,
Nawe huendi pamoja na
majeshi yetu.
- 10 Unaendelea kutufanya
tumkimbie adui yetu;^e
Wale wanaotuchukia
wanachukua chochote
wanachotaka.
- 11 Unatutia mikononi mwao
ili tunyafuliwe kama
kondoo;
Umetutawanya miongoni
mwa mataifa.^f
- 12 Unawauza watu wako kwa
bei ya chini kabisa;^g
Hupati faida yoyote kwa
kuwauza.*
- 13 Unatufanya kuwa shutu-
ma kwa majirani wetu,
Kitu cha kudhihakiwa na
kufanyiwa mzaha na
wale wote wanaotuzu-
nguka.
- 14 Unatufanya kuwa kitu cha

44:4 *Au "Toa." #Au "wokovu mkuu."
44:12 *Au "kutokana na bei yao."

SURA YA 44

a Zb 18:39
Flp 4:13

b Zb 60:12

c 1Sa 17:45
Zb 20:7
Zb 33:16

d Yos 24:8

e Kum 28:15, 25

f Kum 28:64

g Kum 32:30

Safu ya 2

a Kum 28:37
2Nya 7:20

b Kut 34:10

c Zb 139:1
Mhu 12:14
Yer 17:10

d Ro 8:36

e Zb 7:6
Zb 78:65, 66

f Ayu 13:24
Zb 13:1
Zb 88:14

- kudharauliwa* miongoni
mwa mataifa,^a
Kitu cha kutikisiwa kichwa
na mataifa.
- 15 Ninaaibika mchana kutwa,
Nami nimelemewa na aibu
yangu,
- 16 Kwa sababu ya sauti za
wale wanaonidhihaki na
kunitukana,
Kwa sababu ya adui yetu
anayelipiza kisasi.
- 17 Tumepatwa na mambo
haya yote, lakini hatuja-
kusahau,
Wala hatujavunja agano
lako.^b
- 18 Moyo wetu haujakenge-
uka;
Hatua zetu hazitoki katika
njia yako.
- 19 Lakini umetuponda maha-
li ambapo mbwamwitu
wanakaa;
Umetufunika kwa kivuli
kizito.
- 20 Ikiwa tumelisahau jina la
Mungu wetu
Au ikiwa tutamnyooshea
mungu wa kigeni mikononi
yetu tunaposali,
- 21 Je, Mungu hatagundua
hilo?
Anajua siri za moyo.^c
- 22 Kwa ajili yako tunauawa
mchana kutwa;
Tumehesabiwa kuwa
kondoo wa kuchinjwa.^d
- 23 Amka. Kwa nini unaende-
lea kulala usingizi, Ee
Yehova?^e
Amka! Usiendeleo kututu-
pa milele.^f
- 24 Kwa nini unauficha uso
wako?

44:14 *Tnn., "methali."

Kwa nini unasahau mateso yetu na kukandamizwa kwetu?

- 25** Kwa maana tumeshushwa chini mavumbini; Miili yetu imegandamizwa ardhini.^a
- 26** Amka utusaidie!^b Tuokoe* kwa sababu ya upendo wako mshikama-nifu.^c

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa "Mayungiyungi." Wa wana wa Kora.^d Maskili.* Wimbo wa upendo.

- 45** Moyo wangu umesisi-muliwa na jambo jema.

Ninasema: "Wimbo wangu unamhusu* mfalme."^e

Ulimi wangu na uwe kalamu^f ya mnakili^g stadi.^g

- 2** Una sura nzuri kuliko wanadamu wote. Maneno yenye fadhili hutiririka kutoka katika midomo yako.^h Ndiyo sababu Mungu amekubariki milele.ⁱ
- 3** Jifunge upanga wako^j pajani, Ee mwenye nguvu,^k Katika heshima na fahari yako.^l
- 4** Na katika fahari yako endelea mpaka ushinde,^{*m} Panda utetee kweli na unyenyekevu na uadilifu,ⁿ Na mkono wako wa kulia utatimiza[#] mambo yana-yoogopesha.

44:26 *Tnn., "Tukomboe." 45:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. 45:1 *Tnn., "Kazi zangu zinamhusu." [#]Au "mwandishi." 45:4 *Au "ufanikiwe." [#]Tnn., "utakufundisha."

SURA YA 44

a Zb 119:25

b Zb 33:20

c Zb 130:7

SURA YA 45

d 2Nya 20:19

e Zb 2:6

f Isa 8:1

g 2Sa 23:2
Ezr 7:6

h Yoh 7:46

i Zb 72:17

j Ufu 1:16
Ufu 19:15

k Isa 9:6

l Ebr 1:3

m Ufu 6:2

n Ufu 19:11

Safu ya 2

a Zb 2:9
2Th 1:7, 8b Ufu 17:14
Ufu 19:19

c Zb 89:29, 36

d Isa 11:4
Yer 33:15
Ebr 1:8, 9

e Ebr 7:26

f Mt 7:23

g Isa 61:1
Mdo 10:38

h Zb 21:6

i Isa 13:12

- 5** Mishale yako ni mikali, inaangusha mataifa mbele yako;^a Inachoma mioyo ya maadui wa mfalme.^b
- 6** Mungu ni kiti chako cha ufalme milele na milele;^c Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya unyoofu.^{*d}
- 7** Ulipenda uadilifu^e na kuchukua uovu.^f Ndiyo sababu Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta^g kwa mafuta ya kushangilia^h kuliko wenzako.
- 8** Mavazi yako yote yame-tiwa manukato ya manemane na udi na kida; Kutoka katika jumba tukufu la mfalme lililote-ngenezwa kwa pembe za tembo, vinanda vinaku-fanya ushangilie.
- 9** Mabinti wa wafalme ni miongoni mwa wanawake wako wanaoheshimiwa. Malkia amesimama mkono wako wa kulia, akiwa amepambwa kwa dhaha-bu ya Ofiri.ⁱ
- 10** Sikiliza, Ee binti, sikiliza kwa makini na utege sikio lako; Wasahau watu wako na nyumba ya baba yako.
- 11** Naye mfalme atautamani urembo wako, Kwa maana yeye ni bwana wako, Kwa hiyo mwinamie.
- 12** Binti ya Tiro ataleta za-wadi; Watu matajiri zaidi watata-futa kibali chako.*

45:6 *Au "haki." 45:12 *Au "watautu-liza uso wako."

13 Katika jumba la mfalme,*
binti ya mfalme ana
utukufu mwingi ajabu;
Mavazi yake yamepambwa
kwa[#] dhahabu.

14 Atapelekwa kwa mfalme
akiwa na mavazi yaliyo-
fumwa kwa ustadi
mkubwa.*

Mabikira wenzake wanao-
mfuata wanaletwa ndani
mbele ya mfalme.

15 Wataletwa kwa furaha na
shangwe;
Wataingia katika jumba la
mfalme.

16 Wana wako watachukua
mahali pa mababu zako.
Utawaweka kuwa wakuu
katika dunia yote.^a

17 Nitalitangaza jina lako
katika vizazi vyote
vijavyo.^b

Ndiyo sababu mataifa
yatakusifu milele na
milele.

Kwa kiongozi. Wa wana wa
Kora.^c Kulingana na mtindo wa
Alamothi.* Wimbo.

46 Mungu ni kimbilio letu
na nguvu zetu,^d
Msaada unaopatikana
kwa urahisi nyakati za
taabu.^e

2 Ndiyo sababu hatutao-
gopa, hata dunia
ikibadilika,
Hata milima ikianguka
katika vilindi vya
bahari,^f

3 Hata maji yake yakingu-
ruma na povu lake
kufurika,^g

45:13 *Tnn., “Ndani.” #Tnn., “yameti-
wa mapambo ya.” **45:14** *Au labda,
“kwa majoho yaliyotariziwa.” **46:Uta**
*Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 45

a Isa 32:1

b Zb 72:17

SURA YA 46

c 2Nya 20:19

d Met 14:26
Isa 25:4e Kum 4:7
Zb 145:18, 19
Nah 1:7

f Isa 54:10

g Zb 93:4
Yer 5:22

Safu ya 2

a 2Nya 6:6

b Kum 23:14
Zb 132:13
Isa 12:6

c Kut 14:24

d Yos 2:24

e Yos 1:9
Yer 1:19
Ro 8:31f Isa 11:9
Mik 4:3

g Isa 2:11

h 1Nya 29:11

i 2Nya 20:17

j Zb 48:3
Zb 125:2

Hata milima ikitikiswa na
msukosuko wake. (*Sela*)

4 Kuna mto ambao vijito
vyake hufanya jiji la
Mungu lishangilie.^a

Hema la ibada la Aliye Juu
Zaidi lililo takatifu na
tukufu.

5 Mungu yuko katika jiji
hilo;^b haliwezi kupindu-
liwa.

Mungu atalisaidia wakati
wa mapambazuko.^c

6 Mataifa yalikuwa katika
msukosuko, falme zilipi-
nduliwa;
Alipaza sauti yake, dunia
ikayeyuka.^d

7 Yehova wa majeshi yuko
pamoja nasi;^e

Mungu wa Yakobo ni
kimbilio letu salama.*
(*Sela*)

8 Njoooni mtazame matendo
ya Yehova,
Jinsi alivyotenda mambo
yanayostaajibisha
duniani.

9 Anakomesha vita katika
dunia yote.^f

Anauvunja upinde na
kuuvunja mkuki
vipandevipande;
Anayateketeza magari ya
vita motoni.*

10 “Salimuni amri na mjue
kwamba mimi ni Mungu.
Nitakwezwa miongoni
mwa mataifa;^g
Nitakwezwa duniani.”^h

11 Yehova wa majeshi yuko
pamoja nasi;ⁱ
Mungu wa Yakobo ni
kimbilio letu salama.^j
(*Sela*)

46:7 *Au “kilele chetu salama.” **46:9**
*Au labda, “Anaziteketeza ngao mo-
toni.”

Kwa kiongozi.

Muziki wa wana wa Kora.^a

47 Enyi mataifa yote, pige-
ni makofi.

Mpigieni Mungu kelele za
ushindi kwa vigelegele
vya shangwe.

2 Kwa maana Yehova, Aliye
Juu Zaidi, ni mwenye
kuogopesha;^b

Yeye ndiye Mfalme mkuu
juu ya dunia yote.^c

3 Huyatiisha mataifa chini
yetu;
Huyaweka mataifa chini ya
miguu yetu.^d

4 Hutuchagua urithi wetu,^e
Fahari ya Yakobo, ambaye
anampenda.^f (*Sela*)

5 Mungu amepanda juu kwa
kelele za shangwe;
Yehova, kwa sauti ya
pembe.*

6 Mwimbieni Mungu sifa,*
mwimbieni sifa.

Mwimbieni sifa Mfalme
wetu, mwimbieni sifa.

7 Kwa maana Mungu ni
Mfalme wa dunia yote;^g
Mwimbieni sifa, na
mwonyeshe ufahamu.

8 Mungu amekuwa Mfalme
juu ya mataifa.^h

Mungu huketi kwenye kiti
chake kitakatifu cha
ufalme.

9 Viongozi wa mataifa wa-
mekusanyika pamoja
Pamoja na watu wa Mungu
wa Abrahamu.

Kwa maana watawala wa
dunia ni wa* Mungu.

Amekwezwa sana.ⁱ

47:5 *Au "pembe ya kondoo dume; tarumbeta." 47:6 *Au "Mpigieni Mungu muziki." 47:9 *Tnn., "ngao za dunia ni za."

SURA YA 47

a 2Nya 20:19

b Zb 76:12

c Zb 22:28

d Kum 33:29

e Kum 9:5

f Kum 7:6
Mal 1:2

g Yer 10:7
Zek 14:9

h 1Nya 16:31
Zb 96:10
Zb 97:1
Ufu 19:6

i Zb 97:9

Safu ya 2

SURA YA 48

a 2Nya 20:19

b Omb 2:15

c Zb 47:8
Zb 135:21
Mt 5:34, 35

d Zb 125:1

e Zb 87:5
Isa 2:2
Mik 4:1

f Zb 26:3
Zb 40:10
Zb 63:3

Wimbo.

Muziki wa wana wa Kora.^a

48 Yehova ni mkuu na ana-
stahili kabisa kusifiwa
Katika jiji la Mungu wetu,
katika mlima wake mta-
katifu.

2 Urefu wake unavutia, sha-
ngwe ya dunia yote,^b
Ni Mlima Sayuni ulio mbali
sana kaskazini,
Jiji la Mfalme Mkuu.^c

3 Katika minara yake yenye
ngome,
Mungu ametangaza kwa-
mba yeye ni kimbilio
salama.*^d

4 Kwa maana tazama! wafal-
me wamekusanyika;*
Wamesonga mbele pa-
moja.

5 Walipoliona, walishangaa.
Wakashikwa na wasiwasi
na kukimbia kwa hofu.

6 Wakaanza kutetemeka wa-
kiwa huko,
Wakashikwa na uchungu
kama wa mwanamke
anayezaa.

7 Kwa upepo wa mashariki
unavunjavunja meli za
Tarshishi.

8 Mambo tuliyosikia, tume-
jionea wenyewe
Katika jiji la Yehova wa
majeshi, katika jiji la
Mungu wetu.

Mungu ataliimarisha kabi-
sa milele.^e (*Sela*)

9 Tunautafakari upendo
wako mshikamanifu,
Ee Mungu,^f
Katika hekalu lako.

10 Kama jina lako, Ee Mungu,
sifa yako

48:3 *Au "kilele salama." 48:4 *Au "wamekutana kama walivyokubaliana."

Hufika mpaka kwenye miisho ya dunia.^a

Mkono wako wa kuume umejaa uadilifu.^b

- 11** Mlima Sayuni^c na ushangilie,
Miji ya Yuda na ishangilie,^{*}
kwa sababu ya hukumu zako.^d
- 12** Pigeni mwendo kuzunguka Sayuni; lizungukeni pande zote;
Hesabuni minara yake.^e
- 13** Wekeni mioyo yenu juu ya maboma yake.^{*f}
Kagueni minara yake yenye ngome,
Ili msimulie vizazi vijavyo kulihusu.
- 14** Kwa maana Mungu huyu ni Mungu wetu^g milele na milele.

Yeye mwenyewe atatuongoza kwa umilele wote.^{*h}

Kwa kiongozi.

Muziki wa wana wa Kora.ⁱ

- 49** Sikieni hili, enyi mataifa yote.
Sikilizeni, enyi wakaaji wote wa ulimwengu,^{*}
- 2** Wakubwa kwa wadogo,^{*}
Matajiri na pia maskini.
- 3** Kinywa changu mwenyewe kitasema maneno ya hekima,
Na kutafakari kwa moyo wangu^j kutaonyesha kwamba nina uelewaji.
- 4** Nitasikiliza methali;
Nitategua kitendawili changu kwa kinubi.

48:11 *Tnn., "Mabinti wa Yuda na washangilie." 48:13 *Au "kuta zake zenye ngome." 48:14 *Au labda, "mpaka tufe." 49:1 *Au "wa mfumo wa mambo." 49:2 *Tnn., "Wana wa wana-damu na pia wana wa mtu."

SURA YA 48

a Zb 113:3

b Zb 17:7
Zb 60:5
Zb 98:2

c Zb 78:68

d Zb 97:8

e Ne 12:38, 39

f Isa 26:1

g Zb 31:14

h Isa 58:11

SURA YA 49

i 2Nya 20:19

j Zb 143:5

Safu ya 2

a Zb 27:1

b Kum 8:17, 18
Met 18:11

c Yer 9:23
1Ti 6:17

d Met 11:4
Mt 16:26

e Zb 89:48

f Mhu 2:16
Ro 5:12

g Zb 39:6
Met 11:4
Met 23:4
Mhu 2:18
Lu 12:19, 20

h Zb 39:5
Yak 1:11

i Zb 49:20

j Lu 12:19, 20

- 5** Kwa nini niogope nyakati za taabu,^a

Ninapozungukwa na uovu wa* wale wanaojaribu kunipindua?

- 6** Wale wanaotumaini mali zao^b

Na kujigamba kuhusu utajiri wao mwingi,^c

- 7** Hakuna yeyote kati yao anayeweza kamwe kumkomboa ndugu yake Wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake,^d

- 8** (Bei ya fidia* kwa ajili ya uhai wao^e ni yenye thamani sana

Hivi kwamba hawawezi kamwe kulipa);

- 9** Ili kwamba aishi milele asilione shimo.^{*e}

- 10** Anaona kwamba hata watu wenye hekima hufa;

Wapumbavu na wasio-tumia akili huangamia pamoja,^f

Nao hulazimika kuwaachia wengine mali zao.^g

- 11** Ndani yao wanatamani nyumba zao zidumu milele,

Mahema yao kizazi baada ya kizazi.

Wameyaita mashamba yao kwa majina yao.

- 12** Lakini mwanadamu, ingawa anaheshimiwa, hataendelea kuishi,^h

Yeye si bora kuliko wanyama wanao-angamia.ⁱ

- 13** Hiyo ndiyo njia ya wapumbavu^j

Na ya wale wanaowafuata,

49:5 *Tnn., "kosa la." 49:8 *Au "ukombozi." #Au "nafsi yao." 49:9 *Au "kaburi."

wanaofurahia maneno
yao yasiyo na maana.
(Sela)

- 14 Kama kondoo, wamepa-
ngiwa kwenda Kaburini.*
Kifo kitawachunga;
Wanyoofu watawatawala^a
asubuhi.
Kila sehemu ya mwili wao
itatoweka kabisa;^b
Kaburi*^c litakuwa makao
yao badala ya jumba la
mfalme.^d
- 15 Lakini Mungu ata-
nikomboa^e kutoka
katika nguvu za^Δ
Kaburi,*^e
Kwa maana atanishika.
(Sela)
- 16 Usiogope mtu anapota-
jirika,
Fahari ya nyumba yake
ikiongezeka,
17 Kwa maana akifa hawezi
kwenda na kitu cho-
chote;^f
Fahari yake haitashuka
shimoni pamoja
naye.^g
- 18 Kwa maana wakati wa
maisha yake anajiponge-
za mwenyewe.^h
(Watu hukusifu unapopata
ufanisi.)ⁱ
- 19 Lakini mwishowe hujiu-
nga na kizazi cha
mababu zake.
Hawataona nuru tena
kamwe.
- 20 Mtu ambaye haelewi
jambo hili, ingawa
anaheshimiwa,^j
Yeye si bora kuliko wanya-
ma wanaoangamia.

49:14, 15 *Au "Sheoli." Angalia Kamu-
si, uku. 2012. 49:15 #Au "ataikomboa
nafsi yangu." ^ΔTnn., "mkono wa."

SURA YA 49

a Mal 4:3

b Zb 39:11

c Ayu 24:19

d 1Sa 2:6
Ayu 7:9e Ayu 33:28
Zb 16:10
Zb 30:3
Zb 86:13f Ayu 1:21
Mhu 5:15
ITI 6:17

g Isa 10:3

h Lu 12:19

i Met 14:20

j Zb 49:12

Safu ya 2

SURA YA 50

a 1Nya 25:1

b Zb 95:3

c Zb 48:2
Omb 2:15

d Isa 65:6

e Kut 19:18
Da 7:9, 10
Ebr 12:29

f Zb 97:3, 4

g Kum 30:19
Kum 32:1
Isa 1:2

h Mik 6:2

i Kut 24:8

j Zb 75:7

k Ne 9:30
Zb 81:8

l Kut 20:2

m 1Sa 15:22
Isa 1:11
Yer 7:22, 23
Ho 6:6Muziki wa Asafu.^a

- 50** Mungu wa miungu,
Yehova,*^b amesema;
Anaiita dunia
Kutoka mapambazuko ya
jua mpaka machweo
yake.[#]
- 2 Kutoka Sayuni, ukamilifu
wa uzuri,^c Mungu hua-
ngaza.
- 3 Mungu wetu atakuja na
hawezi kunyamaza.^d
Mbele zake kuna moto
unaoteketeza kabisa,^e
Na dhoruba kali inamzu-
nguka pande zote.^f
- 4 Anaziita mbingu zilizo juu
na pia dunia,^g
Ili awahukumu watu
wake.^h
- 5 "Nikusanyieni washikama-
nifu wangu,
Wale wanaofanya agano
pamoja nami kwa
dhabihu."ⁱ
- 6 Mbingu zinatangaza uadi-
lifu wake,
Kwa maana Mungu mwe-
nyewe ni Mwamuzi.^j
(Sela)
- 7 "Sikilizeni, enyi watu
wangu, nami nitaongea;
Israeli, nitatoa ushahidi
dhidi yako.^k
Mimi ni Mungu, Mungu
wako.^l
- 8 Siwakaripii kwa sababu ya
dhabihu zenu,
Wala kwa sababu ya dha-
bihi zenu nzima za
kuteketezwa ambazo
daima ziko mbele
zangu.^m
- 9 Sihitaji kuchukua ng'o-
mbe dume katika
nyumba yako,

50:1 *Au "Yule Mungu, Yehova." #Au
"Kutoka mashariki mpaka magharibi."

Wala mbuzi* katika mazizi yako.^a

- 10** Kwa maana kila mnyama wa mwituni ni wangu,^b Hata wanyama walio juu ya milima elfu moja.
- 11** Ninamjua kila ndege wa milimani;^c Wanyama wasio na idadi wa mbugani ni wangu.
- 12** Ninge kuwa na njaa, nisi- ngekwambia, Kwa maana nchi inayozaa na kila kitu kilichomo ni changu.^d
- 13** Je, nitakula nyama ya ng'ombe dume Na kunywa damu ya mbuzi?^e
- 14** Toa shukrani zikiwa dha- bihu yako kwa Mungu,^f Na utimize nadhiri zako kwa Aliye Juu Zaidi;^g
- 15** Nililie wakati wa taabu.^h Nitakuokoa, nawe utanitu- kuza."ⁱ
- 16** Lakini Mungu atamwa- mbia mwovu: "Una haki gani ya kusimu- lia masharti yangu^j Au kuongea kuhusu agano langu?^k
- 17** Kwa maana unachukua ni- dhamu,* Nawe unaendelea kuya- geuzia mgongo maneno yangu."^l
- 18** Unapomwona mwizi, una- pendezwa naye,^m Nawe unashirikiana na wa- zinzi.
- 19** Unatumia kinywa chako kueneza mabaya,

50:9 *Tnn., "mbuzi dume." 50:17 *Au "mafundisho." ^aTnn., "kuyatupa ma- neno yangu nyuma yako." 50:18 *Au labda, "unaungana naye."

SURA YA 50

- a Mik 6:7
b 1Nya 29:14
Mdo 17:24
c Ayu 38:41
d Kum 10:14
Ayu 41:11
1Ko 10:26
e Mik 6:6-8
f Zb 69:30, 31
Met 21:3
Ho 6:6
Ebr 13:15
g Kum 23:21
Zb 76:11
Mhu 5:4
h 2Nya 33:12, 13
Zb 91:15
i Zb 22:21-23
Zb 50:23
j Yer 7:4
Mt 7:22, 23
Ro 2:21
k Kum 31:20
Ebr 8:9
l Ne 9:26
Isa 5:24
m Isa 5:22, 23

Safu ya 2

- a Yer 9:5
b Law 19:16
c Zb 50:4
Mhu 12:14
d Zb 9:17
Yer 2:32
Ho 4:6
e 1Th 5:18
Ebr 13:15
f Mik 6:8

SURA YA 51

- g 2Sa 11:3
h Hes 14:18
Zb 25:7
Zb 41:4
i Zb 103:13
Met 28:13
Isa 43:22
Isa 44:22
j Isa 1:18
1Ko 6:11
k Ebr 9:13, 14
1Yo 1:7

Na udanganyifu umeshika- mana na ulimi wako.^a

- 20** Unaketi na kumsema vibaya ndugu yako mwenyewe;^b Unafunua makosa ya* mwana wa mama yako mwenyewe.
- 21** Ulipofanya mambo hayo, niliendelea kunyamaza, Kwa hiyo ukafikiri kwa- mba nitakuwa kama wewe. Lakini sasa nitakukaripia, Nami nitatangaza kesi yangu dhidi yako.^c
- 22** Tafadhali, zingatieni jambo hili, ninyi mnao- msahau Mungu,^d Nisije nikawararua vi- pandevipande asiwepo yeyote wa kuwaokoa.
- 23** Yule anayetoa shukrani kuwa dhabihu yake ana- nitukuza,^e Na yule anayefuata njia iliyowekwa, Nitamfanya aone wokovu wa Mungu."^f

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi, nabii Nathani alipokuja kwake baada ya Daudi kulala na Bath-sheba.^g

51 Ee Mungu, nionyeshe kibali kulingana na upendo wako mshika- manifu.^h

Yafute kabisa makosa yangu kulingana na rehema zako nyingi.ⁱ

- 2** Nioshe kabisa kutoka katika kosa langu,^j Na unisafishe kutoka katika dhambi yangu.^k
- 3** Kwa maana ninajua vizuri makosa yangu,

50:20 *Au "Unamharibia sifa."

Na dhambi yangu iko
mbele yangu* daima.^a

- 4 Dhidi yako wewe—wewe
zaidi ya wote*—nimete-
nda dhambi;^b

Nimetenda yaliyo mabaya
machoni pako.^c

Kwa hiyo, wewe ni mwadi-
lifu unapongea,
Wewe ni mwenye haki kati-
ka hukumu yako.^d

- 5 Tazama! Nilizaliwa nikiwa
na hatia ya kosa,
Na mama yangu alini-
chukua mimba katika
dhambi.*^e

- 6 Tazama! Unapendezwa na
ukweli katika utu wa
ndani;^f
Ufundishe utu wangu wa
ndani kabisa* hekima ya
kweli.

- 7 Nisafishe kutoka katika
dhambi yangu kwa
hisopo, ili niwe safi;^g
Nioshe, ili niwe mweupe
kuliko theluji.^h

- 8 Acha nisikie sauti za sha-
ngwe na furaha,
Ili mifupa uliyoiponda
ishangilie.ⁱ

- 9 Ugeuze uso wako* mbali
na dhambi zangu,^j
Na uyafutilie mbali# mako-
sa yangu yote.^k

- 10 Umba moyo safi ndani
yangu, Ee Mungu,^l
Na uweke roho mpya ndani
yangu,^m iliyo imara.

- 11 Usinitupe kutoka mbele
zako*;

51:3 *Au "akilini mwangu." 51:4 *Tnn., "wewe peke yako." 51:5 *Au "Na niliku-
wa na dhambi tangu mama yangu alipo-
nichukua mimba." 51:6 *Au "utu wan-
gu wa sirini." 51:9 *Au "Ufiche uso
wako." #Au "uyafute kabisa." 51:11
*Tnn., "mbele za uwepo wako."

SURA YA 51

a Zb 32:5
Zb 40:12

b Mwa 39:9
2Sa 12:13

c 2Sa 12:9
Zb 38:18

d Ro 3:4

e Ayu 14:4
Ro 3:23
Ro 5:12

f 1Sa 16:7
2Fa 20:3
1Nya 29:17

g Law 14:3, 4
Ebr 9:13, 14

h Isa 1:18

i Zb 6:2
Zb 38:3
Isa 57:15

j Zb 103:12
Isa 38:17

k Mik 7:19

l Yer 32:39

m Eze 11:19
Efe 4:23

Safu ya 2

a Zb 21:1

b Mdo 2:38

c Mwa 9:6

d Zb 38:22
Isa 12:2
Ufu 7:10

e Ne 9:33
Zb 35:28
Zb 59:16
Da 9:7

f Zb 34:1
Zb 109:30
Ebr 13:15

g Met 21:3

h 1Sa 15:22
Zb 40:6
Ho 6:6

i 2Fa 22:18, 19
2Nya 33:13
Zb 22:24
Zb 34:18
Met 28:13
Isa 57:15
Lu 15:22-24
Lu 18:13, 14

j Ho 14:2

Wala usiniondolee roho
yako takatifu.

- 12 Nirudishie shangwe ya
wokovu wako;^a

Chochea ndani yangu
utayari wa kukutii.*

- 13 Nitawafundisha wakosaji
njia zako,^b
Ili watenda dhambi waku-
rudie.

- 14 Niokoe kutoka katika
hatia ya damu,^c Ee Mu-
ngu, Mungu wa wokovu
wangu,^d

Ili ulimi wangu utangaze
uadilifu wako kwa
shangwe.^e

- 15 Ee Yehova, ifungue mido-
mo yangu,
Ili kinywa changu kitanga-
ze sifa yako.^f

- 16 Kwa maana hutaki dhabi-
hu—la sivyo ningeitoa;^g
Hupendezwi na dhabihu
nzima ya kuteketezwa.^h

- 17 Dhabihu zinazompendeza
Mungu ni roho iliyo-
vunjika;
Moyo uliovunjika na
kupondeka, Ee Mungu,
hutaokataa.*ⁱ

- 18 Kwa nia yako njema lite-
ndee jiji la Sayuni jambo
jema;
Zijenge kuta za Yeru-
salemu.

- 19 Ndipo utakapopendezwa
na dhabihu za uadilifu,
Dhabihu za kuteketezwa
na matoleo mazima;
Kisha ng'ombe dume
watatolewa kwenye
madhabahu yako.^j

51:12 *Tnn., "Nitegemeze kwa kunipa
roho ya utayari." 51:17 *Au "hutau-
dharau."

Kwa kiongozi. Maskili.*
 Wa Daudi, Doegi Mwedomu
 alipokuja na kumwambia Sauli
 kwamba Daudi alikuwa ameenda
 kwenye nyumba ya Ahimeleki.^a

52 Kwa nini unajigamba
 kuhusu matendo yako
 maovu, ewe mwenye
 nguvu?^b

Upendo mshikamanifu wa
 Mungu unadumu mcha-
 na kutwa.^c

2 Ulimi wako, wenye makali
 kama wembe,^d

Hupanga madhara na ku-
 tunga mambo ya
 udanganyifu.^e

3 Unapenda uovu kuliko
 mema,

Kusema uwongo kuliko
 kusema ukweli. (*Sela*)

4 Unapenda kila neno lina-
 lodhuru,

Ewe ulimi mdanganyifu!

5 Ndiyo sababu Mungu
 atakubomoa milele na
 milele;^f

Atakunyakua na kukura-
 rua kutoka katika hema
 lako;^g

Atakung'oa kutoka katika
 nchi ya walio hai.^h (*Sela*)

6 Waadilifu wataona jambo
 hilo na kujawa na woga,ⁱ
 Nao watamcheka.^j

7 "Huyu ndiye mwanamume
 ambaye hakumfanya
 Mungu kuwa kimbilio
 lake,^{*k}

Lakini alikutumaini utajiri
 wake mwingi^l

Na kutegemea[#] njama
 zake mwenyewe za
 uovu."^Δ

52:Uta; 53:Uta *Angalia Kamusi,
 uku. 2012. 52:7 *Au "ngome yake."
[#]Au "kujificha katika." ^ΔTnn., "taabu
 anazosababisha."

SURA YA 52

a 1Sa 22:9

b 1Sa 21:7
Zb 94:3, 4

c Zb 103:17

d Zb 57:4
Zb 59:7e 1Sa 22:9, 18
Zb 109:2f Met 12:19
Met 19:9

g Zb 37:9

h Met 2:22

i Zb 37:34

j Zb 58:10

k Yer 17:5

l Zb 49:6, 7
Met 11:28

Safu ya 2

a Zb 13:5
Zb 147:11

b Zb 50:15

c Zb 27:14
Zb 123:2
Met 18:10

SURA YA 53

d Zb 10:4
Ro 1:21e Zb 14:1-7
Ro 3:10f Zb 11:4
Zb 33:13-15
Yer 16:17
Yer 23:24g 1Nya 28:9
2Nya 15:2
2Nya 19:1, 3
Isa 55:6
1Pe 3:12h Mhu 7:20
Ro 3:12

i Ayu 21:7, 14

8 Lakini mimi nitakuwa
 kama mzeituni wenye
 majani mengi katika
 nyumba ya Mungu;
 Ninautumaini upendo
 mshikamanifu wa Mu-
 ngu,^a milele na milele.

9 Nitakusifu milele kwa sa-
 babu umechukua hatua;^b
 Mbele ya washikamanifu
 wako,

Nitalitumaini jina lako,^c
 kwa maana ni jema.

Kwa kiongozi; katika mtindo wa
 Mahalathi.* Maskili.* Wa Daudi.

53 Mpumbavu* husema
 moyoni mwake:

"Hakuna Yehova."^d

Matendo yao maovu yame-
 potoka na yanachukiza;
 Hakuna yeyote anayete-
 nda mema.^e

2 Lakini Mungu anawata-
 zama wanadamu kutoka
 mbinguni^f

Ili aone ikiwa kuna yeyote
 aliye na ufahamu, ikiwa
 kuna yeyote anayemta-
 futa Yehova.^g

3 Wote wamekengeuka;
 Wote wamepotoka.

Hakuna yeyote anayete-
 nda mema,

Hakuna hata mmoja.^h

4 Je, hakuna mtenda maovu
 yeyote anayeelewa?

Wanawala watu wangu
 kwa pupa kana kwamba
 wanakula mkate.

Hawamwiti Yehova.ⁱ

5 Lakini watajawa na hofu
 kubwa,

Hofu ambayo hawajawahi
 kamwe kuwa nayo,^{*}

53:1 *Au "Asiye na akili." 53:5 *Au lab-
 da, "Hofu mahali pasipo na chochote
 cha kuhofu."

Kwa maana Mungu atai-tawanya mifupa ya wale wanaowashambulia ninyi.*

Mtawaibisha, kwa maana Yehova amewakataa wao.

6 Laiti wokovu wa Israeli ungetoka Sayuni!^a

Yehova anapowakusanya tena watu wake walio-tekwa,

Yakobo na ashangilie, Israeli na afurahi.

Kwa kiongozi; uimbwe kwa vinanda. Maskili.* Wa Daudi, Wazifu walipokuja na kumwambia Sauli: “Daudi anajificha miongoni mwetu.”^b

54 Ee Mungu, niokoe kwa jina lako,^c

Na unitetea*^d kwa nguvu zako.

2 Ee Mungu, isikie sala yangu;^e

Sikiliza maneno ya kinywa changu.

3 Kwa maana wageni wanainuka dhidi yangu,

Na wanaume wakatili wanatafuta uhai wangu.*^f

Hawamheshimu Mungu.*^g (*Sela*)

4 Tazama! Mungu ni msaidizi wangu;^h

Yehova yuko pamoja na wale wanaonitegemeza.

5 Utawalipa maadui wanguⁱ uovu wao wenyewe;

Katika uaminifu wako, waangamize.*^j

53:5 *Tnn., “wanaopiga kambi dhidi yenu.” 54:Uta; 55:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. 54:1 *Au “uamue kesi yangu.” 54:3 *Au “nafsi yangu.” *Au “Hawamweki Mungu mbele yao.” 54:5 *Tnn., “wanyamazishe.”

SURA YA 53

a Isa 12:6

SURA YA 54

b 1Sa 23:19
1Sa 26:1

c Zb 20:1
Zb 79:9
Met 18:10

d Zb 43:1

e Zb 13:3
Zb 65:2

f Zb 22:16
Zb 59:3

g Zb 36:1

h 1Nya 12:18
Ebr 13:6

i Ro 12:19

j Zb 143:12

Safu ya 2

a Zb 50:14
Ebr 13:15

b Zb 7:17
Zb 52:9

c 2Sa 4:9
Zb 34:19
Zb 37:39

d Zb 37:34
Zb 59:10

SURA YA 55

e 1Pe 3:12

f Zb 28:2
Zb 143:7

g Zb 17:1

h Isa 38:14

i 2Sa 16:5-7

j Zb 69:29

k Zb 18:4
Zb 116:3
Isa 38:10

l 2Sa 15:14

m 1Sa 23:14

6 Nitakutolea dhabihu^a kwa hiari.

Nitalisifu jina lako, Ee Yehova, kwa maana ni jema.^b

7 Kwa maana wewe hunio-koa kutoka katika kila taabu,^c

Nami nitawatazama maadui wangu wakishindwa.^d

Kwa kiongozi; uimbwe kwa vinanda. Maskili.*
Wa Daudi.

55 Sikiliza sala yangu, Ee Mungu,^e

Na usiipuuzze sala yangu ya kuomba rehema.*^f

2 Nisikilize na unijibu.^g Hangaiko langu linanisu- mbua,^h

Nami nimefadhaika

3 Kwa sababu ya mambo ambayo adui anasema Na mkazo kutoka kwa mwovu.

Kwa maana wananirundi- kia taabu,

Na kwa hasira wana chuki kali kunielekea.ⁱ

4 Moyo wangu una maumi- vu makali,^j Na hofu ya kifo inanile- mea.^k

5 Hofu na kutetemeka hunijia, Na woga hunishika.

6 Daima ninasema: “Laiti ningekuwa na mabawa kama ya njiwa! Ningeruka mbali na kukaa kwa usalama.

7 Tazama! Ningekimbia na kwenda mbali sana.^l Ningekaa nyikani.^m (*Sela*)

55:1 *Au “Na usijifiche ninaposali ku-kuomba msaada.”

- 8** Ningeenda haraka mahali pa kujificha Mbali na upepo mkali, mbali na dhoruba.”
- 9** Wavuruge, Ee Yehova, na uvuruge mipango yao,*^a Kwa maana nimeona ukatili na mizozo jijini.
- 10** Usiku na mchana wanazunguka juu ya kuta zake; Ndani yake kuna fitina na taabu.^b
- 11** Uharibifu uko ndani yake; Ukandamizaji na udanganifu hauondoki kamwe katika uwanja wake.^c
- 12** Kwa maana si adui anayenidhihaki;^d La sivyo ningevumilia. Si adui aliyeinuka dhidi yangu; La sivyo ningeweza kujificha.
- 13** Lakini ni wewe, mwanadamu kama mimi,*^e Rafiki yangu mwenyewe ninayemjua vizuri.^f
- 14** Tulikuwa tukifurahia pamoja urafiki wa karibu sana; Katika nyumba ya Mungu tulikuwa tukitembea pamoja na umati.
- 15** Na wapatwe na maangamizi!^g Na washuke Kaburini* wakiwa hai; Kwa maana uovu hukaa miongoni mwao na ndani yao.
- 16** Lakini mimi, nitamlilia Mungu, Na Yehova ataniokoa.^h
- 17** Jioni na asubuhi na adhu-

55:9 *Tnn., “ugawanye ndimi zao.” 55:13 *Au “mwanadamu, mtu tunayelingana.” 55:15 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 55

a 2Sa 15:31
2Sa 17:7

b 2Sa 17:1

c Zb 109:2

d Zb 41:9
Mt 26:21
Yoh 13:18

e 2Sa 15:12
2Sa 16:23

f Lu 22:21
Lu 22:48

g 2Sa 17:23
2Sa 18:14
Zb 109:15
Mt 27:3, 5
Mdo 1:16, 18

h Zb 91:15

Safu ya 2

a Zb 119:147
Da 6:10

b Zb 5:3

c 2Nya 32:7
Zb 3:6

d Zb 143:12

e Kum 33:27
Zb 90:2

f Zb 36:1

g 2Sa 15:12

h 2Sa 5:3
Mhu 8:2

i 2Sa 16:23

j Zb 28:3
Zb 62:4

k Zb 43:5
1Pe 5:6, 7

l Zb 37:5
Zb 68:19
Flp 4:6, 7

m Zb 37:23, 24
Zb 62:2
Zb 121:3

n Zb 55:15

o Zb 5:6
Met 10:27

huri, ninahangaika na kulia kwa uchungu,*^a Naye huisikia sauti yangu.^b

- 18** Ataniokoa* na kunipa amani mbali na wale wanaopigana nami, Kwa maana umati huja kunishambulia.^c
- 19** Mungu atasikia na kukabiliana nao,^d Yule anayeketi kwenye kiti cha ufalme tangu zamani.^e (*Sela*) Watakataa kubadilika, Wale ambaa hawajamwogopa Mungu.^f
- 20** Aliwashambulia* walio na amani pamoja naye;^g Alilivunja agano lake.^h
- 21** Maneno yake ni laini kuli-ko siagi,ⁱ Lakini mzozo umo moyoni mwake. Maneno yake ni laini kuli-ko mafuta, Lakini ni panga zilizocho-molewa.^j
- 22** Mtupie Yehova mzigo wako,^k Naye atakutegemeza.^l Hataruhusu kamwe mwadilifu aanguke.*^m
- 23** Lakini wewe, Ee Mungu, utawashusha chini kwenye shimo lenye kina kabisa.ⁿ Watu hao wenye hatia ya damu ambao ni wadangananyifu hawataishi nusu ya siku zao.^o Lakini mimi, nitakutumai ni wewe.

55:17 *Au “nimevurugika.” 55:18 *Tnn., “Atanikomboa.” 55:20 *Yaani, rafiki yake wa zamani anayetajwa katika mstari wa 13 na 14. 55:22 *Au “ayumbeyumbe; apeesuke.”

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa “Njiwa Mnyamavu Aliye Mbali.” Wa Daudi. Miktamu.*

Wafilisti walipomkamata kule Gathi.^a

56 Nionyeshe kibali, Ee Mungu, kwa sababu mwanadamu anayeweza kufa ananishambulia.*

Mchana kutwa wanaendelea kunipiga vita na kunikandamiza.

2 Maadui wangu wanajaribu mchana kutwa kuni-ng’ata;

Wengi wanapigana nami kwa kiburi.

3 Ninapoooga,^b ninakutumaini wewe.^c

4 Katika Mungu—ninayelisi-fu neno lake—

Katika Mungu ninaweka tumaini langu; siogopi.

Mwanadamu ambaye ni duni tu atanifanya* nini?^d

5 Mchana kutwa wanavuruga mambo yangu; Jambo pekee wanalowazia ni kunidhuru.^e

6 Wanajificha ili wanishambulie, Wanachunguza kila hatua yangu,^f

Wakikusudia kuuondoa uhai wangu.^g

7 Wakatae kwa sababu ya uovu wao.

Yaangushe mataifa kwa hasira yako, Ee Mungu.^h

8 Unafuatia kutangatanga kwangu.ⁱ Yakusanye machozi yangu katika kiriba chako cha ngozi.^j

56:Uta; 57:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. 56:1 *Au “anataka kuni-ng’ata.” 56:4 *Tnn., “Mwili wa nyama utanifanya.”

SURA YA 56

a 1Sa 21:10

b 1Sa 21:12

c Zb 18:2

d Zb 27:1
Zb 56:10, 11
Ro 8:31
Ebr 13:6

e Yer 18:18

f Lu 20:20

g Zb 59:3
Zb 71:10

h Yer 18:23

i 1Sa 27:1

j Zb 39:12

Safu ya 2

a Mal 3:16

b Zb 18:40

c Ro 8:31

d Zb 27:1

e Zb 56:4
Isa 51:7, 12

f Hes 30:2
Mhu 5:4

g Zb 50:23

h 2Ko 1:10

i Zb 94:18
Zb 116:8

j Ayu 33:29, 30

SURA YA 57

k 1Sa 22:1
1Sa 24:3
Zb 142:Uta

l Zb 18:2

m Ru 2:12

Zb 17:8

n Zb 144:7
Mdo 12:11

Je, hayajaandikwa katika kitabu chako?^a

9 Maadui wangu watakimbia siku nitakayoomba msaada.^b

Nina hakika kuhusu jambo hili: Mungu yuko upande wangu.^c

10 Katika Mungu—ninayelisi-fu neno lake— Katika Yehova—ninayelisi-fu neno lake—

11 Katika Mungu ninaweka tumaini langu; siogopi.^d Mwanadamu ambaye ni duni tu atanifanya nini?^e

12 Nimefungwa na nadhiri nilizokuwekea, Ee Mungu;^f Nitakutolea matoleo ya shukrani.^g

13 Kwa maana umeniokoa kutoka katika kifo,^h Na kuizuia miguu yangu isijikwae,ⁱ Ili nitembee mbele za Mungu katika nuru ya walio hai.^j

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa “Usiharibu.” Wa Daudi. Miktamu.* Alipomkimbia Sauli na kuingia pangoni.^k

57 Nionyeshe kibali, Ee Mungu, nionyeshe kibali,

Kwa maana ninakukimbilia,^l

Ninakimbilia kivuli cha mabawa yako mpaka matatizo haya yapite.^m

2 Ninamlilia Mungu Aliye Juu Zaidi,

Mungu wa kweli, anayeyakomesha kwa ajili yangu.

3 Atatuma msaada kutoka mbinguni na kuniokoa.ⁿ

Atamtamausha yule anayejaribu kuning’ata. (Sela)

Mungu atatuma upendo wake mshikamanifu na uaminifu wake.^a

4 Nimezungukwa na simba;^b

Nimelazimika kulala miongoni mwa watu wanaotaka kuninyafua, Ambao mena yao ni miku-ki na mishale

Na ambao ulimi wao ni upanga mkali.^c

5 Ukwezwe juu ya mbingu, Ee Mungu;

Utukufu wako na uwe juu ya dunia yote.^d

6 Wameutayarisha wavu ili kuinasa miguu yangu;^e

Taabu zimenifanya niina-me chini.^f

Wamechimba shimo mbele yangu,

Lakini wao wenyewe wameanguka ndani yake.^g (*Sela*)

7 Moyo wangu uko imara, Ee Mungu,^h

Moyo wangu uko imara. Nitaimba na kupiga muziki.

8 Amka, utukufu wangu. Amka, Ee kinanda; nawe pia, Ee kinubi.

Nitayaamsha mapambazuko.ⁱ

9 Nitakusifu miongoni mwa mataifa, Ee Yehova;^j

Nitakuambia sifa* miongoni mwa mataifa.^k

10 Kwa maana upendo wako mshikamanifu ni mku-bwa, uko juu kama mbingu,^l

Na uaminifu wako, unafika mpaka angani.

11 Ukwezwe juu ya mbingu, Ee Mungu;

57:9 *Au "Nitakupigia muziki."

SURA YA 57

a Zb 40:11
Zb 61:7

b Zb 22:13
Zb 35:17

c Zb 52:2
Zb 64:3
Met 25:18

d Zb 57:11
Zb 108:5

e Zb 35:7

f Zb 42:6

g 1Sa 24:4
Met 26:27

h Zb 112:7

i Zb 108:2-5

j Zb 9:11
Zb 145:11, 12

k Ro 15:9

l Zb 36:5
Zb 103:11

Safu ya 2

a Zb 8:1
Zb 57:5
Zb 108:5

SURA YA 58

b 2Nya 19:6

c Zb 82:2

d Mhu 3:16
Mik 3:9

e Mhu 5:8
Isa 10:1, 2

f Zb 140:3
Yak 3:8

Utukufu wako na uwe juu ya dunia yote.^a

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa "Usiharibu." Wa Daudi. Miktamu.*

58 Je, mnaweza kuzungu-mza kuhusu uadilifu wakati mmenyamaza?^b

Je, mnaweza kuhukumu kwa unyoofu, enyi wana-damu?^c

2 Badala yake, mnatunga uovu moyoni mwenu,^d

Na mikonu yenu inatawanya ukatili nchini.^e

3 Waovu wanakengeuka* tangu kuzaliwa;

Ni wakaidi, waongo tangu wanapozaliwa.

4 Sumu yao ni kama sumu ya nyoka;^f

Wao ni viziwi kama swila anayeziba sikio lake.

5 Hataisikiliza sauti ya wanaomchezeshu,

Hata wafanye uchawi kwa ustadi kadiri gani.

6 Ee Mungu, yavunje meno yao vinywani mwao!

Yavunje mataya ya hawa simba,* Ee Yehova!

7 Na watoweke kama maji yanayotiririka na kwen-nda zake.

Mungu na aukunje upinde wake na kuwaangusha kwa mishale yake.

8 Na wawe kama konokono anayeyeyuka anapote-mbea;

Kama mtoto anayefia tu-mboni mwa mwanamke, mtoto asiyeona jua kamwe.

58:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.

58:3 *Au "wamepotoka." 58:6 *Au "wanasimba wenye manyoya marefu shingoni."

- 9 Kabla vyungu vyenu vya kupikia havijapata moto wa kuni za mkwamba, Atazifagilia mbali kuni zenye unyevu na zinazowaka moto, kama kwa kimbunga.^a
- 10 Mwadilifu atashangilia kwa sababu ameona kisasi;^b Miguu yake italowa damu ya waovu.^c
- 11 Kisha watu watasema: “Kwa hakika kuna thawabu kwa ajili ya mwadilifu.^d Kwa hakika kuna Mungu anayehukumu duniani.”^e
- Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa “Usiharibu.” Wa Daudi. Miktamu. * Sauli alipowatuma watu waichunguze nyumba ya Daudi^f ili wamuue.^f
- 59** Niokoe kutoka kwa maadui wangu, Ee Mungu wangu;^g Nilinde kutoka kwa wale wanaoinuka dhidi yangu.^h
- 2 Niokoe kutoka kwa wale wanaotenda uovu, Na uniokoe kutoka kwa watu wakatili. *
- 3 Tazama! Wanavivizia;ⁱ Wanaume wenye nguvu wanishambulia Lakini si kwa sababu nimeasi au kutenda dhambi,^j Ee Yehova.
- 4 Ingawa sikutenda kosa lolote, wanakimbia na kujitayarisha kunishambulia. Inuka ninapokuita, uone.
- 5 Kwa maana wewe, Ee Ye-

59:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Tnn., “waichunguze ile nyumba.” 59:2 *Au “wenye kiu ya damu.”

SURA YA 58

a Met 10:25
Yer 23:19

b Zb 52:5, 6
Zb 64:10
Eze 25:17
Ufu 18:20

c Met 21:18

d Isa 3:10

e Zb 9:16
Zb 98:9

SURA YA 59

f 1Sa 19:11

g 1Sa 19:12
Zb 18:48
Zb 71:4

h Zb 12:5
Zb 91:14

i 1Sa 19:1
Zb 10:9
Zb 71:10

j 1Sa 24:11
1Sa 26:18
Zb 69:4

Safu ya 2

a Kum 33:29

b Met 2:22

c 1Sa 19:11

d Zb 22:16

e Zb 59:14

f Zb 57:4
Zb 64:3

g Zb 10:4, 11
Zb 73:3, 11

h Zb 37:12, 13

i Zb 33:10

j Zb 27:1
Zb 46:1

k Zb 9:9
Zb 62:2

l Zb 6:4

m Zb 54:7

n Mwa 15:1
Kum 33:29
Zb 3:3

o Zb 64:8
Met 12:13
Met 16:18

hova Mungu wa majeshi, ni Mungu wa Israeli.^a Amka uyakazie uangalifu mataifa yote.

Usiwaonyeshe rehema wasaliti wowote wenye nia ya kudhuru.^b (Sela)

6 Wanarudi kila jioni;^c Wanabweka* kama mbwa^d na kuzungukazunguka jijini.^e

7 Tazama kinachomwagika* kutoka katika kinywa chao;

Midomo yao ni kama panga,^f

Kwa maana wanauliza: “Ni nani anayesikiliza?”^g

8 Lakini wewe, Ee Yehova, utawacheka;^h Utayadhikahi mataifa yote.ⁱ

9 Ee Nguvu zangu, nitaendelea kukutarajia;^j Kwa maana Mungu ni kimbilio langu salama.*^k

10 Mungu anayenitendea kwa upendo mshikamanifu atanisaidia;^l Mungu ataniwezesha niwatazame maadui wangu wakishindwa.^m

11 Usiwaue, ili watu wangu wasisahau.

Kwa nguvu zako wafanye watangetange; Waangushe, Ee Yehova, ngao yetu.ⁿ

12 Kwa sababu ya dhambi ya kinywa chao, neno la midomo yao, Kiburi chao na kiwanase,^o Kwa sababu ya matusi na udanganyifu wanaosema.

59:6 *Au “Wananguruma.” 59:7 *Au “kinachobubujika.” 59:9 *Au “kilele changu salama.”

13 Waangamize kwa hasira yako kali;^a
 Waangamize kabisa, ili wasiwepo tena;
 Wafanye wajue kwamba Mungu anatawala katika Yakobo na mpaka kwenye miisho ya dunia.^b
(Sela)

14 Acha warudi jioni;
 Acha wabweke* kama mbwa na kuzungukazunguka jijini.^c

15 Acha watangetange wakitafuta chakula;^d
 Usiwaruhusu washibe au kupata makao.

16 Lakini mimi, nitaimba kuhusu nguvu zako;^e
 Asubuhi nitatangaza kwa shangwe kuhusu upendo wako mshikamanifu.

Kwa maana wewe ni kimbilio langu salama^f
 Na mahali pangu pa kukiimbilia wakati wa taabu.^g

17 Ee Nguvu zangu, nitakuiambia sifa,^{*h}
 Kwa maana wewe Mungu ni kimbilio langu salama, Mungu unayenitendea kwa upendo mshikamanifu.ⁱ

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa “Yungiyungi la Kikumbusho.” Miktamu.* Wa Daudi. Wa kufundisha.

Alipopigana na Aram-naharaimu na Aram-Soba, kisha Yoabu akarudi na kuwaua Waedomu 12,000 katika Bonde la Chumvi.^j

60 Ee Mungu, ulitukataa; ulipenya katika vikosi vyetu vya ulinzi.^k
 Ulitukasirikia; lakini sasa tupokee tena!

59:14 *Au “wanguume.” 59:17 *Au “nitakupigia muziki.” 60:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 59

a Zb 7:9

b 1Sa 17:46
Zb 9:16
Zb 83:17, 18

c Zb 59:6

d Zb 109:2, 10

e Ayu 37:23
Zb 21:13
Zb 145:10-12f 1Sa 17:37
Zb 61:3

g Met 18:10

h Isa 12:2

i Zb 59:10

SURA YA 60

j 2Sa 8:13
1Nya 18:3

k Zb 60:10

Safu ya 2

a Isa 51:17

b Zb 18:35
Zb 21:8
Zb 108:6
Zb 118:15
Isa 41:10

c Mwa 12:6, 7

d Yos 13:27, 28
Zb 108:7-9

e Yos 13:29-31

f Mwa 49:10

g Hes 24:17
2Sa 8:2h Hes 24:18
2Sa 8:14

i 2Sa 8:1

j 2Sa 8:14
Zb 108:10-13

2 Uliifanya dunia itetemeke; uliipasua ikafunguka. Ziba nyufa zake, kwa maana inaporomoka.

3 Uliwafanya watu wako wateseke.
 Ulitufanya tunywe divai inayofababisha tuyumbeyumbe.^a

4 Wape* ishara wale wanakuogopa
 Wakimbie na kuukwepa upinde. *(Sela)*

5 Ili wapendwa wako waokolewe,
 Tuokoe kwa mkono wako wa kuume na utujibu.^b

6 Mungu ameongea katika utakatifu wake.*
 “Nitashangilia, nitawagawia Shekemu kuwa urithi,^c

Nami nitawapimia Bonde la[#] Sukothi.^d

7 Gileadi ni yangu, na Manasse ni yangu,^e
 Na Efraimu ni kofia ya kuinga* kichwa changu;
 Yuda ni fimbo yangu ya kiongozi.^f

8 Moabu ni beseni langu la kuogea.^g
 Nitatupa kiatu changu juu ya Edomu.^h

Nitapaza sauti kwa ushindi juu ya Ufilisti.ⁱ

9 Ni nani atakayenipeleka kwenye jiji lililozingirwa?^{*j}

Ni nani atakayeniongoza mpaka Edomu?^j

10 Je, si wewe, Ee Mungu, ambaye umetukataa,

60:4 *Au labda, “Umewapa.” 60:6 *Au labda, “mahali pake patakatifu.”
 #Au “Nchi Tambarare ya Chini ya.”
 60:7 *Tnn., “ngome ya.” 60:9 *Au labda, “lenye ngome.”

Mungu wetu, ambaye haendi tena na majeshi yetu?^a

- 11 Tusaidie katika taabu yetu,
Kwa maana wokovu kuto-
ka kwa wanadamu hauna
faida yoyote.^b

- 12 Kwa msaada wa Mungu
tutapata nguvu,^c
Naye atawakanyagia chini
maadui wetu.^d

Kwa kiongozi; uimbwe kwa
vinanda. Wa Daudi.

- 61** Ee Mungu, sikia kilio
changu cha kuomba
msaada.

Sikiliza sala yangu.^e

- 2 Nitakulilia kwa sauti
kutoka katika miisho
ya dunia

Ninapovunjika moyo.^{*f}

Niongoze kwenye mwamba
ulio juu kuliko mimi.^g

- 3 Kwa maana wewe ni ki-
mbilio langu,
Mnara ulio imara unaonili-
nda dhidi ya adui.^h

- 4 Nitakuwa mgeni katika
hema lako milele;ⁱ
Nitakimbilia katika kivuli
cha mabawa yako.^j (*Sela*)

- 5 Kwa maana wewe, Ee Mu-
ngu, umesikia nadhiri
zangu.

Umenipa urithi wa wale
wanaoliogopa jina lako.^k

- 6 Utamwongezea mfalme
siku za maisha yake,^l
Na miaka yake itatoka ki-
zazi hadi kizazi.

- 7 Ataketi kwenye kiti cha
ufalme* milele mbele za
Mungu;^m

Mpe upendo wako mshika-

61:2 *Au "Moyo wangu unapodhoofika."

61:7 *Au "Atakaa."

SURA YA 60

a Kum 1:42
Kum 20:4
Yos 7:12

b Zb 62:9
Zb 118:8
Zb 146:3

c Zb 18:32

d 2Sa 10:12
Zb 44:5

SURA YA 61

e Zb 5:2
Zb 17:1
Zb 28:2
Zb 55:1

f Yon 2:2

g Zb 27:5
Zb 40:2

h 1Sa 17:45
Zb 18:2
Met 18:10

i Zb 23:6
Zb 27:4

j Zb 63:7

k Zb 115:13

l Zb 18:50
Zb 21:1, 4

m 2Sa 7:16, 17
Zb 41:12

Safu ya 2

a Zb 40:11
Zb 143:12
Met 20:28

b Zb 146:2

c Zb 65:1
Zb 66:13
Mhu 5:4

SURA YA 62

d Zb 37:39
Zb 68:19
Isa 12:2

e Zb 18:2

f Zb 37:23, 24
2Ko 4:8, 9

g Zb 38:12

h Zb 5:9
Zb 28:3
Zb 55:21

i Zb 43:5
Mik 7:7

j Zb 62:1, 2
Zb 71:5

manifu na uaminifu, ili
vimlinde.^a

- 8 Kisha nitaliambia sifa* jina
lako milele^b

Ninapotimiza nadhiri za-
ngu siku baada ya siku.^c

Kwa kiongozi; wa Yeduthuni.*
Muziki wa Daudi.

- 62** Kwa kweli, ninamngojea
Mungu kimyakimya.

Wokovu wangu unatoka
kwake.^d

- 2 Kwa kweli, yeye ni mwa-
mba wangu na wokovu
wangu, kimbilio langu
salama;^{*e}

Kamwe, sitatikiswa sana.^f

- 3 Mtaendelea mpaka lini
kumshambulia mtu ili
kumuua?^g

Ninyi nyote ni hatari kama
ukuta ulioinama, ukuta
wa mawe unaokaribia
kuanguka.*

- 4 Kwa maana wanashau-
riana ili kumwangusha
kutoka katika cheo
chake cha juu;*

Wanafurahia kusema
uwongo.

Kwa kinywa chao wana-
bariki, lakini ndani yao
wanalaani.^h (*Sela*)

- 5 Kwa kweli, ninamngojea*
Mungu kimyakimyaⁱ

Kwa sababu tumaini langu
linatoka kwake.^j

- 6 Kwa kweli, yeye ni mwa-
mba wangu na wokovu

61:8 *Au "nitalipigia muziki." 62:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. 62:2 *Au "kilele changu salama." 62:3 *Au lab-
da, "Ninyi nyote, kana kwamba alikuwa
ukuta ulioinama, ukuta wa mawe unao-
karibia kuanguka." 62:4 *Au "heshima
yake." 62:5 *Au "Kwa kweli, Ee nafsi
yangu, mngojee."

wangu, kimbilio langu salama;

Sitatikiswa kamwe.^a

- 7 Wokovu wangu na utukufu wangu unamtegemea Mungu.

Mwamba wangu imara, kimbilio langu, ni Mungu.^b

- 8 Mtumainini nyakati zote, enyi watu.

Mwageni mioyo yenu mbele zake.^c

Mungu ni kimbilio letu.^d (Sela)

- 9 Wanadamu ni pumzi tu, Wana wa binadamu ni njozi ya uwongo.^e

Wanapowekwa pamoja kwenye mizani, ni wepesi kuliko pumzi.^f

- 10 Msitegemee upunjaji Wala kuwa na matumaini ya uwongo katika unyang'anyi.

Mali zako zikiongezeka, usizikazie moyoni mwako.^g

- 11 Mungu ameongea mara moja, mara mbili nimelisikia jambo hili:

Kwamba nguvu ni za Mungu.^h

- 12 Pia upendo mshikamanifu ni wako, Ee Yehova,ⁱ

Kwa maana unamlipa kila mtu kulingana na mateendo yake.^j

Muziki wa Daudi, alipokuwa katika nyika ya Yuda.^k

- 63** Ee Mungu, wewe ni Mungu wangu, ninaindelea kukutafuta.^l

Nina kiu kwa ajili yako.^m

Ninazimia* kwa sababu ninakutamani

Katika nchi kame iliyokauka, ambayo haina maji.ⁿ

63:1 *Tnn., "Mwili wangu unazimia."

SURA YA 62

a Zb 16:8
Met 10:30

b Zb 95:1
Isa 26:4

c 1Sa 1:15

d Met 14:26

e Zb 60:11

f Isa 40:15

g Kum 6:10-12
Ayu 31:24, 28
Met 11:4, 28
Met 23:4, 5
Mt 6:19, 24
Mk 8:36
Lu 12:15
1Ti 6:17
1Yo 2:16

h Ayu 9:4
Nah 1:3
Ufu 19:1

i Zb 36:7
Zb 86:15
Mik 7:18

j Ayu 34:11
Met 24:12
Ro 2:6
2Ko 5:10
Gal 6:7
2Ti 4:14
Ufu 20:12, 13
Ufu 22:12

SURA YA 63

k 1Sa 23:14

l Isa 26:9

m Zb 42:2

n Zb 63:Uta
Zb 143:6

Safu ya 2

a 1Nya 16:28
Zb 96:6

b Zb 30:5
Zb 100:5

c Zb 66:16, 17

d Zb 71:23
Zb 135:3

e Zb 119:55, 148

f 1Sa 17:37

g Zb 5:11
Zb 57:1
Zb 61:4

h Isa 41:10

- 2 Kwa hiyo nimekutazama mahali patakatifu; Nimeziona nguvu zako na utukufu wako.^a

- 3 Kwa sababu upendo wako mshikamanifu ni bora kuliko uhai,^b Midomo yangu mwenyewe itakutukuza.^c

- 4 Basi nitakusifu maisha yangu yote; Katika jina lako nitaiinua mikono yangu.

- 5 Nimeridhika na fungu bora ambalo ni zuri kabisa,*

Kwa hiyo kinywa changu kitakusifu kwa midomo yenye shangwe.^d

- 6 Ninakukumbuka wewe ni-kiwa kitandani mwangu; Ninatafakari kukuhusu katika makesha ya usiku.^e

- 7 Kwa maana wewe ni msaidizi wangu,^f

Nami ninapaza sauti kwa shangwe katika kivuli cha mabawa yako.^g

- 8 Ninashikamana nawe; Mkono wako wa kuume hunishika kwa nguvu.^h

- 9 Lakini wale wanaotaka kuniua*

Watashuka katika sehemu zenye kina zaidi za dunia.

- 10 Watatiwa katika nguvu za upanga;

Watakuwa chakula cha mbwamwitu.*

- 11 Lakini mfalme atashangilia kwa sababu ya Mungu.

63:5 *Tnn., "Nimeridhika kana kwamba nina mafuta na nimejaa mafuta." 63:9 *Au "kuiangamiza nafsi yangu." 63:10

*Au "mbweha."

Kila mtu anayeapa katika jina la Mungu atashangilia,*

Kwa maana kinywa cha wale wanaosema uwongo kitanyamazishwa.

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

64 Ee Mungu, sikia sauti yangu ninapokusihia.^a Ulinde uhai wangu kutokana na hofu ya adui.

2 Nikinge kutokana na njama za siri za waovu,^b Kutoka kwa umati wa watenda movu.

3 Wanaunoa ulimi wao kama upanga; Wanayalenga maneno yao ya ukatili kama mishale,

4 Ili wampige mtu asiye na hatia wakiwa mafichoni; Wanampiga ghafla, bila kuogopa.

5 Wanashikamana sana na kusudi lao oву,* Wanazungumzia jinsi ya kuficha mitego yao.

Wanasema: "Ni nani atakayeiona?"^c

6 Wanatafuta njia mpya za kutenda uovu; Wanatunga kwa siri mbinu zao za ujanja;^d

Fikira zilizo ndani ya moyo wa kila mmoja wao hazieleweki kamwe.

7 Lakini Mungu atawapiga mishale;^e Watajeruhiwa kwa ghafla na mshale.

8 Ulimi wao wenyewe utasababisha waanguke;^f Wote wanaowatazama watatikisa kichwa.

9 Ndipo watu wote wataogopa,

63:11 *Au "atajigamba." 64:5 *Au "Wanatia moyo kutenda uovu."

SURA YA 64

a Zb 55:1

b Zb 56:6
Zb 109:2

c Zb 10:4, 11
Zb 59:7

d Zb 140:5

e Zb 7:11, 12

f Met 12:13
Met 18:7

Safu ya 2

a Zb 107:40, 43

b Zb 58:10
Zb 68:2, 3

SURA YA 65

c Zb 76:2

d Zb 116:18
Mhu 5:4

e Zb 145:18
Mdo 10:31
1Yo 5:14

f Zb 40:12
Ro 7:23, 24
Gal 5:17

g Zb 51:2
Isa 1:18
1Yo 1:7

h Zb 15:1-5
Zb 27:4
Zb 84:1-4
Zb 84:10

i Zb 36:7, 8

j 1Sa 3:3
1Nya 16:1

k Kum 10:21
Ufu 15:3

l Zb 22:27

m Zb 93:1

n Zb 89:9
Zb 107:29

Nao watatangaza mambo ambayo Mungu ametenda,

Nao watayafahamu matendo yake.^a

10 Mwadilifu atashangilia kwa sababu ya Yehova na kumkimbilia;^b

Wote walio wanyoofu moyoni watashangilia.*

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi. Wimbo.

65 Ee Mungu, sifa inakungojea Sayuni;^c Tutatimiza nadhiri zetu kwako.^d

2 Ee Msikiaji wa sala, watu wa kila aina* watakuja.^e

3 Dhambi zangu zimenilemea,^f Lakini unafunika makosa yetu.^g

4 Mwenye furaha ni yule unayemchagua na kumleta karibu Ili akae katika nyua zako.^h Tutaridhika na wema wa nyumba yako,ⁱ Hekalu lako takatifu.^j

5 Utatujibu kwa matendo ya uadilifu yanayogopesha,^k Ee Mungu wa wokovu wetu;

Wewe ndiye Tegemeo la miisho yote ya dunia^l Na wa wale walio mbali ng'ambo ya bahari.

6 Uliimarisha kabisa milima kwa nguvu zako; Umevaa uwezo.^m

7 Unazituliza bahari zilizo-chafuka,ⁿ Kishindo cha mawimbi

64:10 *Au "watajigamba." 65:2 *Tnn., "watu wote wenye mwili." 65:4 *Au "Mahali pako patakatifu."

yake na msukosuko wa mataifa.^a

- 8 Wale wanaokaa sehemu za mbali wataogopesha na ishara zako;^b

Utawafanya wale wanaoishi upande wa mashariki mpaka upande wa magharibi wapaze sauti kwa shangwe.

- 9 Unaitunza dunia, Unafanya izee kwa wingi* na kuitajirisha sana.^c

Kijito kinachotoka kwa Mungu kimejaa maji; Unawapa nafaka,^d Kwa maana hivyo ndivyo ulivyoitayarisha dunia.

- 10 Unajaza maji katika mitaro yake na kusawazisha udongo wake uliolimwa;* Unailainisha kwa manyonyu ya mvua; unabariki mimea yake.^e

- 11 Unauvika mwaka taji kwa wema wako; Vijia vyako vinafurika kwa wingi wa vitu.^{*f}

- 12 Malisho ya nyikani yanaendelea kufurika,^{*g} Na vilima vimevishwa shangwe.^h

- 13 Malisho yamefunikwa na makundi ya kondoo, Na mabonde yamefunikwa* na nafaka.ⁱ Yanapaza sauti kwa ushindi, naam, yanaimba.^j

Kwa kiongozi. Wimbo. Muziki.

- 66** Mpazieni Mungu sauti ya ushindi, dunia yote.^k

65:9 *Tnn., "ifurike." 65:10 *Au "matuta yake." 65:11 *Tnn., "vinadondosha mafuta." 65:12 *Tnn., "kudondosha." 65:13 *Au "nchi tambarare za chini zimefunikwa."

SURA YA 65

a Isa 17:12, 13
Isa 57:20

b Zb 66:3

c Kum 11:11, 12
Mdo 14:17

d Zb 104:14, 15

e Zb 147:7, 8

f Mwa 27:28
Kum 33:16
Mal 3:10

g Isa 35:1

h Isa 55:12

i Isa 30:23

j Mdo 14:17

SURA YA 66

k Zb 98:4

Safu ya 2

a Zb 72:19
Ufu 4:11

b Kut 15:16
Zb 76:12
Isa 2:19
Yer 10:10

c Zb 81:15

d Zb 22:27
Mal 1:11

e Isa 42:10
Ufu 15:4

f Zb 46:8
Sef 2:11

g Kut 14:21, 22

h Yos 3:15, 16

i Kut 15:1

j Da 4:34
1Ti 1:17

k Zb 11:4
Met 15:3
Ebr 4:13

l Isa 37:29

m Kum 32:43
Ro 15:10

n 1Sa 25:29

o Isa 2:9
Zb 121:3

p Kum 8:2

- 2 Liimbieni sifa* jina lake tukufu.

Tukuzeni sifa yake.^a

- 3 Mwambieni Mungu: "Kazi zako zinaogopesha kwelikweli!"^b

Kwa sababu ya nguvu zako nyingi,

Maadui wako watajikunyata mbele zako.^c

- 4 Dunia yote itakuinamia;^d Watakuimbia sifa; Wataliimbia sifa jina lako."^e (*Sela*)

- 5 Njoooni mwone kazi za Mungu.

Mambo aliyowatendea wanadamu yanaogopesha.^f

- 6 Aliigeuza bahari kuwa nchi kavu;^g

Walivuka mto kwa miguu.^h Huko tulishangilia kwa sababu yake.ⁱ

- 7 Anatawala milele/ kwa nguvu zake.

Macho yake yanachunguza mataifa.^k

Wale ambao ni wakaidi hawapaswi kujikweza.^l (*Sela*)

- 8 Msifuni Mungu wetu, enyi mataifa,^m

Sauti ya sifa yake na isikiwe.

- 9 Yeye hutuhifadhi hai;^{*n} Haruhusu miguu yetu jikwae.^{#o}

- 10 Kwa maana umetuchunguza, Ee Mungu;^p

Umetusafisha kama fedha inavyosafishwa.

- 11 Ulituingiza katika wavu wa kuwindia;

Ulitutwika mzigo mzito.*

66:2 *Au "Lipigieni muziki." 66:9 *Au "Hufanya nafsi zetu kuwa hai." #Au "iyumbeyumbe; itetemeke." 66:11 *Tnn., "Uliweka mzigo mzito kwenye viuno vyetu."

12 Ulimruhusu mwanadamu anayeweza kufa apande juu yetu;*

Tulipita motoni na katika maji;

Kisha ukatuleta mahali penye kitulizo.

13 Nitaingia katika nyumba yako nikiwa na dhabihu nzima za kuteketezwa;^a

Nitatimiza nadhiri zangu kwako^b

14 Ambazo midomo yangu iliahidi^c

Na kinywa changu kili-sema nilipokuwa katika taabu.

15 Nitakutolea dhabihu za kuteketezwa za wanyama waliononeshwa Pamoja na moshi wa dhabihu za kondoo dume.

Nitatoa ng'ombe dume pamoja na mbuzi dume. (*Sela*)

16 Njooi msikilize, ninyi nyote mnaomwogopa Mungu,

Nami nitawaambia mambo aliyonitendea.^d

17 Nilimwita kwa kinywa changu

Na kumtukiza kwa ulimi wangu.

18 Ikiwa nilihifadhi moyoni mwangu jambo lolote linalodhuru,

Yehova hangenisikia.^e

19 Lakini Mungu alinisikia;^f Aliisikiliza sala yangu.^g

20 Asifiwe Mungu, ambaye hakukataa sala yangu Wala kuninyima upendo wake mshikamanifu.

SURA YA 66

a Hes 15:3

b Zb 56:12
Zb 116:14
Mhu 5:4, 5

c Hes 30:2
Amu 11:35

d Zb 22:24

e Ayu 27:8, 9
Met 15:29
Met 28:9
Isa 1:15
Yoh 9:31

f Zb 34:6
Zb 65:2
Zb 116:1
1Yo 3:22

g Ebr 5:7

Safu ya 2

SURA YA 67

a Hes 6:25
Met 16:15

b Ro 10:18
Kol 1:23

c Zb 98:2
Isa 49:6
Lu 2:30, 31
Mdo 28:28
Tit 2:11

d Isa 42:10

e Zb 9:8
Zb 96:10
Zb 98:9
Ro 2:5

f Law 26:4
Zb 85:12
Isa 30:23
Eze 34:27

g Mwa 17:7

h Zb 22:27
Ufu 15:4

SURA YA 68

i Hes 10:35
Zb 21:8

j Nah 1:6

Kwa kiongozi; uimbwe kwa vinanda. Muziki. Wimbo.

67 Mungu atatuonyesha kibali na kutubariki; Atatuangazia nuru ya uso wake^a (*Sela*)

2 Ili njia yako ijulikane duniani kote,^b

Matendo yako ya wokovu miongoni mwa mataifa yote.^c

3 Mataifa na yakusifu wewe, Ee Mungu;

Mataifa yote na yakusifu.

4 Mataifa na yashangilie na kupaza sauti kwa shangwe,^d

Kwa maana utayahukumu mataifa kwa haki.^e

Utayaongoza mataifa ya dunia. (*Sela*)

5 Mataifa na yakusifu, Ee Mungu;

Mataifa yote na yakusifu wewe.

6 Dunia itatoa mazao yake;^f Mungu, Mungu wetu,

atatubariki.^g

7 Mungu atatubariki, Na miisho yote ya dunia itamwogopa* yeye.^h

Kwa kiongozi. Wa Daudi. Muziki. Wimbo.

68 Mungu na ainuke, maadi wake na watawanyike,

Wale wanaomchukia na wakimbie kutoka mbele zake.ⁱ

2 Wapeperushe mbali kama moshi unavyopeperushwa;

Kama nta inavyoyeyuka karibu na moto,

Waovu na waangamie vi-vyo hivyo kutoka mbele za Mungu.^j

66:12 * Tnn., "juu ya vichwa vyetu."

67:7 * Au "itamheshimu."

- 3** Lakini waadilifu na washangilie;^a
Na wafurikwe na shangwe mbele za Mungu;
Na wafurahi na kushangilia.
- 4** Mwimbieni Mungu; liimbieni sifa* jina lake.^b
Mwimbieni Yule anayepanda kupitia jangwa tambarare.[#]
Jina lake ni Yah!^{Δc} Shangilieni mbele zake!
- 5** Baba wa mayatima na mlinzi* wa wajane^d
Ni Mungu katika makao yake matakatifu.^e
- 6** Mungu huwapa makao walio peke yao;^f
Huwaachilia huru wafungwa na kuwafanikisha.^g
Lakini ni lazima watu wakaidi* waishi katika nchi iliyokauka.^h
- 7** Ee Mungu, ulipowaongoza* watu wako,ⁱ
Ulipopiga mwendo jangwani, (*Sela*)
- 8** Dunia ilitetemeka;^j
Mbingu zilinyesha* mvua kwa sababu ya Mungu;
Huu Mlima Sinai ulitetemeka kwa sababu ya Mungu, Mungu wa Israeli.^k
- 9** Ulisababisha mvua kubwa inyeshe, Ee Mungu;
Uliwatia nguvu tena watu wako waliochoka.*
- 10** Walikaa katika kambi yako yenye mahema;^l

68:4 *Au "lipigieni muziki." [#]Au labda, "juu ya mawingu." ^Δ"Yah" ni ufupisho wa jina Yehova. **68:5** *Tnn., "mwa-muzi." **68:6** *Au "waasi." **68:7** *Tnn., "ulipotangulia mbele ya." **68:8** *Tnn., "zilidondosha." **68:9** *Tnn., "Uliuita nguvu tena urithi wako."

SURA YA 68

a Zb 32:11

b Isa 12:4

c Kut 6:3

d Kut 22:22-24
Kum 10:17, 18
Zb 10:14
Zb 146:9

e Isa 57:15

f Zb 113:9

g Isa 61:1

h Kum 28:15, 23
Zb 107:33, 34i Kut 13:21
j Zb 114:1, 4
Ebr 12:26
k Kut 19:18
Amu 5:4, 5
l Hes 10:34

Safu ya 2

a Kut 15:20
Amu 5:1
Amu 11:34
1Sa 18:6b Hes 31:25-27
Yos 10:12, 16
Yos 12:7
Amu 5:19c Hes 31:27
1Sa 30:23-25d Hes 21:3
Yos 10:5, 10e Hes 21:33
Kum 3:8, 10f 1Nya 11:5
Zb 48:2, 3
Zb 132:13g Kum 12:5, 6
1Fa 9:3
Ebr 12:22h 2Fa 6:16, 17
Mt 26:53

Kwa wema wako, uliwaandalia maskini, Ee Mungu.

- 11** Yehova anatoa amri;
Wanawake wanaotangaza habari njema ni jeshi kubwa.^a
- 12** Wafalme na majeshi yao wanakimbia,^b wanakimbia!
Mwanamke anayebaki nyumbani anagawiwa nyara.^c
- 13** Ingawa ninyi wanaume mlikuwa mkilala katikati ya mioto kambini,*
Kutakuwa na mabawa ya njiwa yaliyofunikwa kwa fedha,
Yenye manyoya ya dhahabu bora.[#]
- 14** Mweza-Yote alipowatawanya wafalme waliokuwa nchini,^d
Theluji ilianguka Salmoni.*
- 15** Mlima wa Bashani^e ni mlima wa Mungu;*
Mlima wa Bashani ni mlima wenye vilele.
- 16** Enyi milima yenye vilele, kwa nini mnautazama kwa wivu,
Mlima ambao Mungu ameuchagua kuwa* makao yake?^f
Kwa kweli, Yehova atakaa huko milele.^g
- 17** Magari ya Mungu ya vita ni makumi ya maelfu, maelfu kwa maelfu.^h
Yehova ametoka Sinai na

68:13 *Au labda, "katikati ya mazizi ya kondoo." [#]Au "yenye mchanganyiko wa rangi ya manjano na kijani kibichi." **68:14** *Au "Ni kana kwamba theluji ilianguka Salmoni." **68:15** *Au "ni mlima mrefu." **68:16** *Au "anatamani uwe."

kuingia mahali patakatifu.^a

18 Ulipanda juu;^b
Ulichukua mateka;
Ulichukua wanaume
kuwa zawadi,^c
Naam, hata walio wakaidi,^d
ili ukae miongoni mwao,
Ee Yah Mungu.

19 Na asifiwe Yehova, anayetubebea mzungu wetu kila siku,^e
Mungu wa kweli wa wokoovu wetu. (*Sela*)

20 Kwetu, Mungu wa kweli ni Mungu anayeokoa;^f
Na Yehova Bwana Mwenye Enzi Kuu huokoa kutoka katika kifo.^g

21 Naam, Mungu atapondaponda vichwa vya maadui wake,
Utosi wenye nywele wa mtu yeyote anayeendelea kuwa na* hatia.^h

22 Yehova amesema: "Nitawarudisha kutoka Bashani;ⁱ
Nitawarudisha kutoka katika vilindi vya bahari,

23 Ili mguu wako ufunikwe na damu^j
Na ulimi wa mbwa wako upate fungu lake kutoka kwa maadui."

24 Wanaona misafara yako, Ee Mungu,
Misafara ya Mungu wangu, Mfalme wangu, inayolingia mahali patakatifu.^k

25 Waimbaji wanatangulia mbele, wanamuziki wanaopiga vinanda wanawafuata;^l
Katikati yao kuna wana-

68:21 *Au "anayetembea katika."

SURA YA 68

^a Kut 19:23
Kum 33:2

^b 2Sa 5:7

^c Efe 4:8, 11

^d Kum 2:36
Kum 7:22

^e Zb 55:22
1Pe 5:6, 7

^f Isa 12:2
Isa 45:17

^g Kum 32:39

^h Zb 55:23
Eze 18:26

ⁱ Hes 21:33

^j Zb 58:10

^k 1Nya 15:25, 28
Zb 24:7

^l 1Nya 15:16
Zb 87:7
Zb 150:3

Safu ya 2

^a Amu 11:34
1Sa 18:6

^b Zb 95:6
Isa 44:2

^c Mwa 49:27
1Sa 9:21

^d Zb 138:8

^e 1Fa 6:1
1Nya 16:1
Ezr 5:14

^f 1Fa 10:10
2Nya 32:23
Zb 72:10

^g Eze 39:18

^h Isa 45:14
Isa 60:5

ⁱ Kum 32:43

wake vijana wakipiga matari.^a

26 Katika umati uliokutani-ka, * msifuni Mungu; Msifuni Yehova, enyi mnaotoka katika Chemchemi ya Israeli.^b

27 Huko Benjamin, ^c aliye mdogo zaidi, anawatiisha,
Pia wakuu wa Yuda pamoja na umati wao wenye kelele,
Wakuu wa Zabuloni, wakuu wa Naftali.

28 Mungu wako ameamuru kwamba utakuwa na nguvu.

Onyesha nguvu zako, Ee Mungu, wewe ambaye umetenda kwa niaba yetu.^d

29 Kwa sababu ya hekalu lako lililo Yerusalemu,^e Wafalme watakuletea zawadi.^f

30 Wakemee wanyama wa mwituni walio kwenye matete,
Kusanyiko la ng'ombe dume^g na ndama wao, Mpaka mataifa yataka-poinama chini yakileta* vipande vya fedha.

Lakini anayatawanya mataifa yanayopenda vita.

31 Vitu vya shaba nyekundu vitaletwa kutoka* Misri;^h Kushi itafanya haraka kumpa Mungu zawadi.

32 Enyi falme za dunia, mwimbieni Mungu,ⁱ Mwimbieni sifa* Yehova, (*Sela*)

68:26 *Tnn., "Katika makusanyiko."

68:30 *Au labda, "yakikanyagia chini."

68:31 *Au labda, "Mabalozzi wata-toka." **68:32** *Au "Mpigieni muziki."

33 Yule anayepanda mbingu ya kale kati ya mbingu.^a
Tazama! Hunguruma kwa sauti yake, sauti yake yenye nguvu.

34 Tambueni nguvu za Mungu.^b
Fahari yake iko juu ya Israeli,
Na nguvu zake ziko angani.*

35 Mungu anaogopesha kuto-ka katika mahali pake patakatifu penye utukufu.^c

Yeye ni Mungu wa Israeli, Anayewapa watu uwezo na nguvu.^d
Asifiwe Mungu.

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa "Mayungiyungi."
Wa Daudi.

69 Niokoe, Ee Mungu, kwa maana maji yanahatarisha uhai wangu.*^e

2 Nimezama chini katika matope yenye kina, mahali pasipo na udongo mgumu.^f

Nimefika katika maji yenye kina,
Na kijito kinachotiririka haraka kimenifagilia mbali.^g

3 Nimechoka kupaza sauti;^h
Koo langu limekauka.
Macho yangu yamechoka nikimngojea Mungu wangu.ⁱ

4 Wale wanaonichukia bila sababu/
Ni wengi sana kuliko nywele za kichwa changu.

Wale wanaotaka kuniangamiza,

68:34 *Tnn., "mawinguni." **69:1** *Au "nafsi yangu."

SURA YA 68

a Zb 104:3

b Zb 96:7

c Zb 47:2
Zb 66:5d Zb 29:11
Isa 40:29-31

SURA YA 69

e Zb 144:7
Omb 3:54
Yon 2:5

f Zb 40:2

g Zb 32:6
Yon 2:3

h Zb 22:2

i Zb 119:82
Zb 119:123
Isa 38:14j Lu 23:22
Yoh 15:24, 25

Safu ya 2

a Zb 22:6
Yer 15:15b Isa 50:6
Mt 26:67
Mt 27:29c Ayu 19:13
Zb 31:11
Yoh 1:11
Yoh 7:5d 1Fa 19:10
Zb 119:139
Mt 21:12, 13
Mk 11:15-17
Yoh 2:13-17

e Ro 15:3

Maadui wangu wenye hila,* wamekuwa wengi. Nililazimishwa kurudisha kitu ambacho sikuiba.

5 Ee Mungu, unajua upumavu wangu,
Na hatia yangu haijafichika mbele zako.

6 Acha wale wanaokutumaini wasiaibishwe kwa sababu yangu,

Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi.

Wale wanaokutafuta na wasifedheheshwe kwa sababu yangu,

Ee Mungu wa Israeli.

7 Ninashutumiwa kwa sababu yako;^a

Aibu imefunika uso wangu.^b

8 Nimekuwa mgeni kwa ndugu zangu,
Mgeni kwa wana wa mama yangu.^c

9 Bidii kwa ajili ya nyumba yako imenila,^d

Na shutuma za wale wanaokushutumuzime-
niangukia.^e

10 Nilipojinyenyekeza* kwa kufunga,^f

Nilishutumiwa kwa sababu hiyo.

11 Nilipoyafanya magunia kuwa mavazi yangu,
Nikawa kitu cha kudhauruliwa nao.*

12 Wale wanaoketi kwenye lango la jiji huzungumza kunihusu,
Na walevi huimba juu yangu katika nyimbo zao.

69:4 *Au "Wale ambao ni maadui wangu bila sababu." **69:10** *Tnn., "Nilipoinyenyekeza nafsi yangu." ^fAu labda, "Nilipolia na kufunga." **69:11** *Tnn., "Nilikuwa methali kwao."

- 13** Lakini sala yangu na iku-fikie,
Ee Yehova, kwa wakati unaofaa.^a
Katika upendo wako mwingi mshikamanifu, Ee Mungu,
Nijibu kwa matendo yako hakika ya wokovu.^b
- 14** Niokoe kutoka katika matope;
Usiache nizame.
Niokoe kutoka kwa wale wanaonichukia
Na kutoka katika maji yenye kina.^c
- 15** Usiache mafuriko yenye kasi yanifagilie mbali,^d
Wala kilindi kinimeze,
Wala kisima kifumbe* kinywa chake juu yangu.^e
- 16** Nijibu, Ee Yehova, kwa maana upendo wako mshikamanifu ni mwema.^f
Nigeukie kulingana na rehema zako nyingi,^g
- 17** Wala usimfiche mtumishi wako uso wako.^h
Nijibu haraka, kwa maana ninataabika.ⁱ
- 18** Nikaribie uniokoe;*
Nikomboe kwa sababu ya maadui wangu.
- 19** Unajua shutuma yangu na aibu yangu na fedheha yangu.^j
Unawaona maadui wangu wote.
- 20** Shutuma imeuvunja moyo wangu, na jeraha haliwezi kuponywa.*
Nilitarajia kuhurumiwa,

69:15 *Au "shimo lifumbe." **69:18** *Au "Ikaribie nafsi yangu uikomboe."
69:20 *Au "nami nimefikia hatua ya kukata tamaa."

SURA YA 69

a Isa 49:8
Ebr 5:7

b Zb 68:20

c Zb 144:7

d Zb 69:2

e Zb 16:10

f Zb 63:3
Zb 109:21

g Zb 25:16

h Zb 27:9
Zb 102:2

i Zb 31:9
Zb 40:13

j Zb 22:6

Safu ya 2

a Zb 142:4

b Ayu 19:14

c Mt 27:34
Mk 15:23

d Mt 27:48
Mk 15:36
Lu 23:36
Yoh 19:29

e Ro 11:9, 10

f Zb 21:9

g Mdo 1:20

h Kut 32:33

i Flp 4:3
Ufu 3:5
Ufu 13:8

j Zb 109:22

lakini sikuhurumiwa hata kidogo,^a

Nilitarajia kupata watu wa kunifariji, lakini sikupata yeyote.^b

21 Lakini walinipa sumu* kuwa chakula,^c

Na wakanipa siki ninywe ili nikate kiu.^d

22 Meza yao na iwe mtego kwao,

Na ufanisi wao uwe kitu cha kuwanasa.^e

23 Acha macho yao yatiwe giza wasiweze kuona,
Na ufanye viuno vyao vite-temeke daima.

24 Wamwagie ghadhabu yako,*

Na hasira yako inayowaka iwapate.^f

25 Kambi yao* na iwe ukiwa; Mahema yao yasiwe na mkaaji yeyote.^g

26 Kwa maana wanamfuatia yule uliyempiga,
Nao huendelea kusimulia kuhusu maumivu ya wale uliowajeruhi.

27 Ongeza hatia zaidi juu ya hatia yao,

Nao wasiwe na fungu lolote katika uadilifu wako.

28 Na wafutwe kutoka katika kitabu cha walio hai,*^h

Na wasiorodheshwe miongoni mwa waadilifu.ⁱ

29 Lakini ninateseka, nami nina maumivu.^j

Ee Mungu, nguvu zako za kuokoa na zinilinde.

30 Nitaliambia sifa jina la Mungu,

69:21 *Au "mmea wenye sumu." **69:24** *Au "hasira yako kali." **69:25** *Au "Kambi yao iliyozingirwa na ukuta." **69:28** *Au "kitabu cha uzima."

Nami nitamtukuza kwa kutoa shukrani.

- 31** Jambo hilo litampendeza Yehova kuliko ng'ombe dume,
Kuliko ng'ombe dume mchanga mwenye pembe na kwato.^a
- 32** Wapole wataona jambo hilo na kushangilia. Mioyo yenu na ihuishwe, ninyi mnaomtafuta Mungu.
- 33** Kwa maana Yehova anawasikiliza maskini,^b Naye hatawadharau watu wake waliotekwa.^c
- 34** Mbingu na dunia na zimsifu,^d Bahari na kila kitu kinachoogelea ndani yake.
- 35** Kwa maana Mungu atalio-koa Sayuni^e Naye atayajenga upya majiji ya Yuda, Nao watakaa humo na kuimiliki.*
- 36** Wazao wa watumishi wake watairithi,^f Na wale wanaolipenda jina lake^g wataishi humo.
Kwa kiongozi.
Wa Daudi, wa kukumbusha.
- 70** Ee Mungu, niokoe; Ee Yehova, njoo haraka unisaidie.^h
- 2** Wale wanaotaka kuniua* Na waaibishwe na kufedheshwa. Wale wanaofurahia msiba wangu Na wakimbie kwa aibu.
- 3** Wale wanaosema: "Aha! Aha!" Na wakimbizwe kwa aibu.

69:35 *Yaani, ile nchi. 70:2 *Au "wanaoitafuta nafsi yangu."

SURA YA 69

a Zb 50:13-15
Ho 14:2

b Zb 10:17
Zb 102:17
Isa 66:2

c Zb 146:7
Isa 61:1
Lu 4:18

d Zb 96:11
Isa 49:13

e Zb 51:18

f Isa 61:9
Isa 66:22

g Zb 91:14
Yak 1:12

SURA YA 70

h Zb 40:13-17

Safu ya 2

a Zb 5:11
Omb 3:25

b Zb 109:22

c Zb 141:1

d Zb 18:2

e Zb 13:3

SURA YA 71

f Zb 25:2
Zb 31:1-3
Isa 45:17
Yer 17:18

g Zb 34:15

h 2Sa 22:2, 3
Zb 18:2
Zb 144:2

i Zb 17:8, 9
Zb 59:1
Zb 140:4
Mt 6:13

j 1Sa 17:45
Yer 17:7

- 4** Lakini acha wale wanao-kutafuta Wafurahi na kushangilia kwa sababu yako.^a Wale wanaopenda mate-ndo yako ya wokovu na waseme daima: "Mungu na atukuzwe!"
- 5** Lakini sina uwezo, nami ni maskini;^b Ee Mungu, tenda haraka kwa niaba yangu.^c Wewe ni msaidizi wangu na mwokozi wangu.^d Ee Yehova, usikawie.^e

71 Nimekukimbilia wewe, Ee Yehova.

- Usiache niabishwe kamwe.^f
- 2** Niokoe na kuninusuru kwa uadilifu wako. Nitegee sikio lako* na uniokoe.^g
- 3** Uwe ngome ya mwamba kwangu Ambamo ninaweza kuingia sikuzote. Toa amri ya kuniokoa, Kwa maana wewe ni jabali langu na ngome yangu.^h
- 4** Ee Mungu wangu, niokoe kutoka mikononi mwa mwovu,ⁱ Kutoka katika makucha ya mkandamizaji asiye-tenda haki.
- 5** Kwa maana wewe ni tu-maini langu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova; Nimekutumaini wewe* tan-gu nilipokuwa kijana.^j
- 6** Nimekutegemea tangu nilipozaliwa;

71:2 *Au "Inama chini na unisikilize."

71:5 *Au "Wewe ni tegemeo langu."

Wewe ndiye uliyenitoa
tumboni mwa mama
yangu.^a

Ninakusifu daima.

7 Nimekuwa kama muujiza
kwa watu wengi,
Lakini wewe ni kimbilio
langu imara.

8 Kinywa changu kimejaa
sifa zako;^b

Mchana kutwa ninasimulia
kuhusu fahari yako.

9 Usinitupe wakati wa
uzee;^c

Usiniache ninapoishiwa na
nguvu.^d

10 Maadui wangu wanasema
mambo mabaya kuni-
husu,

Na wale wanaotaka
kuniua* wanapanga
njama pamoja,^e

11 Wakisema: "Mungu ame-
mwacha.

Mkimbizeni na kumkama-
ta, kwa maana hakuna
yeyote wa kumwokoa."^f

12 Ee Mungu, usiendelee
kukaa mbali nami.

Ee Mungu wangu, njoo
haraka unisaidie.^g

13 Wale wanaonipinga

Na waaibishwe na kua-
ngamia.^h

Wale wanaonitakia msiba
Na wafunikwe na aibu na
fedheha.ⁱ

14 Lakini mimi, nitaendelea
kungoja;

Nitakusifu hata zaidi.

15 Kinywa changu kitasimu-
lia uadilifu wako,^j

Mchana kutwa kitasimulia
matendo yako ya
wokovu,

71:10 *Au "wanaoitafuta nafsi yangu."

SURA YA 71

a Zb 22:9, 10
Zb 139:16
Isa 46:3

b Zb 51:15
Ebr 13:15

c Zb 92:14

d Zb 73:26
Mhu 12:3

e 2Sa 17:1, 2

f Zb 3:2
Zb 42:10
Mt 27:42, 43

g Zb 22:11
Zb 35:22
Zb 38:21, 22

h 2Sa 17:23

i Zb 109:29

j Zb 35:28
Zb 40:9

Safu ya 2

a Zb 40:5

b Zb 71:5

c 2Sa 22:1
1Nya 16:4
Zb 9:1

d Zb 37:25
Zb 71:9

e Kut 13:8
1Nya 29:10, 11
Zb 78:2-4

f Zb 36:6

g Kut 15:11
Zb 86:8
Zb 89:6
Yer 10:7

h 2Sa 12:10, 11

i Zb 40:2
Zb 86:13

j Zb 25:10
Zb 108:4
Zb 146:6

Ingawa ni mengi sana kwa-
ngu kuyajua.^{*a}

16 Nitakuja na kutangaza
matendo yako yenye
nguvu,

Ee Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova;

Nitatangaza uadilifu wako,
wako peke yako.

17 Ee Mungu, umenifundisha
tangu nilipokuwa
kijana,^b

Na mpaka sasa ninaende-
lea kutangaza kazi zako
zinazostaajibisha.^c

18 Ee Mungu, hata nikizeeka
na kuwa na mvi, usinia-
che.^d

Acha nikiambie kizazi kija-
cho kuhusu nguvu zako*

Na kuwaambia wote
watakaokuja kuhusu
uwezo wako.^e

19 Uadilifu wako, Ee Mungu,
unafika vileleni;^f

Umetenda mambo makuu;
Ee Mungu, ni nani aliye
kama wewe?^g

20 Ingawa umenifanya nipate
taabu nyingi na misiba
mingi,^h

Nihuishe tena;

Niinue kutoka katika
sehemu zenye kina za*
dunia.ⁱ

21 Ongeza ukuu wangu
Nizunguke na kunifariji.

22 Kisha nitakusifu kwa zeze
Kwa sababu ya uaminifu
wako, Ee Mungu wangu.^j

Nitaimba sifa zako* kwa
kinubi,

Ee Mtakatifu wa Israeli.

23 Midomo yangu itapaza

71:15 *Au "kuyahesabu." 71:18 *Tnn.,
"mkono wako." 71:20 *Au "vilindi vya."

71:22 *Au "Nitakupigia muziki."

sauti kwa shangwe nina-
pokuimbia sifa,^a

Kwa maana umeokoa uhai
wangu.*^b

- 24** Ulimi wangu utaongea*
kuhusu uadilifu wako
mchana kutwa,^c

Kwa maana wale wanao-
taka kuniangamiza
wataabishwa na kufe-
dheheshwa.^d

Zaburi Inayomhusu Sulemani.

- 72** Ee Mungu, mpe mfalme
hukumu zako,

Na umzawadie mwana wa
mfalme uadilifu wako.^e

- 2** Na atetee kesi ya watu
wako kwa uadilifu,
Na ya watu wako wa hali ya
chini kwa haki.^f

- 3** Milima na iwalettee watu
amani,
Na vilima vilete uadilifu.

- 4** Na awalinde* watu wa hali
ya chini miongoni mwa
mataifa,

Na awaokoe watoto* wa
mtu maskini,
Na amponde mpunjaji.^g

- 5** Watakuogopa maadamu
jua lipo
Na maadamu mwezi
unadumu,

Kizazi baada ya kizazi.^h

- 6** Atakuwa kama mvua
inayonyeshea majani
yaliyofyekwa,
Kama manyunyu ya mvua
yanayoinyesha dunia.ⁱ

- 7** Katika siku zake mwadili-
fu atasitawi,*^j

Na amani itakuwa nyingi^k
mpaka mwezi utakapo-
kuwa haupo tena.

SURA YA 71

a Zb 63:5
Zb 104:33

b 2Sa 4:9
Zb 103:4

c Zb 71:8

d Zb 71:13

SURA YA 72

e 1Nya 22:11, 12
1Nya 29:19
Yer 23:5

f 1Fa 3:9, 28

g Isa 11:4

h Zb 89:36, 37
Lu 1:32, 33
Ufu 11:15

i 2Sa 23:3, 4
Met 16:15
Met 19:12

j Isa 61:11

k 1Fa 4:25
1Nya 22:9
Isa 2:4
Isa 9:6

Safu ya 2

a Kut 23:31
1Fa 4:21
Zb 2:8
Zb 22:27, 28
Da 2:35
Zek 9:10

b Zb 2:9
Zb 110:1

c 1Fa 4:21

d 1Fa 10:1, 2

e 1Fa 10:10

f Isa 30:23

g Isa 35:1, 2

- 8** Atakuwa na raia* kutoka
bahari mpaka bahari
Na kutoka Mto Efrati mpa-
ka kwenye miisho ya
dunia.^a

- 9** Wakaaji wa jangwani
watainama chini mbele
yake,
Na maadui wake watara-
mba mavumbi.^b

- 10** Wafalme wa Tarshishi
na wa visiwa watalipa
ushuru.^c

Wafalme wa Sheba na wa
Seba watatoa zawadi.^d

- 11** Wafalme wote watainama
chini mbele yake,
Na mataifa yote yatamtu-
mikia.

- 12** Kwa maana atamwoko
maskini anayelilia
msaada,
Pia mtu wa hali ya chini
na yeyote ambaye hana
msaidizi.

- 13** Atamhurumia mtu wa hali
ya chini na maskini,
Naye ataokoa uhai wa*
maskini.

- 14** Atawaokoa* kutoka katika
ukandamizaji na ukatili,
Na damu yao itakuwa na
thamani machoni pake.

- 15** Na aishi na kupewa dha-
habu ya Sheba.^e
Sala na zitolewe daima
kwa ajili yake,
Na abarikiwe mchana
kutwa.

- 16** Kutakuwa na nafaka
nyingi duniani;^f
Itafurika juu ya milima.
Matunda yake yatasitawi
kama ya Lebanoni,^g
Na katika majiji watu

71:23 *Au "umeikomboa nafsi yangu."

71:24 *Au "utatafakari." 72:4 *Tnn.,
"awahukumu." #Au "wana." 72:7
*Tnn., "atachipuka."

72:8 *Au "Atatawala." 72:13 *Au
"nafsi za." 72:14 *Au "Atazikomboa
nafsi zao."

- watachanua kama mi-me-a ya dunia.^a
- 17** Jina lake na lidumu milele,^b
Na lisitawi maadamu jua lipo.
Watu na wajipatie baraka kupitia yeye;^c
Mataifa yote na yamtanga-ze kuwa mwenye furaha.
- 18** Na asifiwe Yehova Mungu, Mungu wa Israeli,^d

SURA YA 72

- a 1Fa 4:20
b Zb 45:17
Zb 89:35, 36
c Mwa 22:18
Gal 3:14
d 1Nya 29:10

Safu ya 2

- a Kut 15:11
b Ufu 5:13
c Hes 14:21
Hab 2:14
d 1Sa 17:58

- Ambaye peke yake hu-tenda mambo yanayostaajibisha.^a
- 19** Jina lake tukufu na lisifi-we milele,^b
Na utukufu wake ujae du-niani pote.^c
Amina na Amina.
- 20** Huo ndio mwisho wa sala za Daudi, mwana wa Yesu.^d

KITABU CHA TATU
(Zaburi 73-89)

- Muziki wa Asafu.^a
- 73** Kwa kweli Mungu ni mwema kwa Israeli, kwa wale walio safi moyoni.^b
- 2** Lakini mimi, miguu yangu ilikuwa karibu kuke-ngeuka;
Hatua zangu zilikuwa kari-bu kuteleza.^c
- 3** Kwa maana niliwaonea wivu wenye kiburi*
Nilipokuwa nikiona amani ya waovu.^d
- 4** Kwa maana hawana mau-mivu wanapokufa;
Miili yao ina afya.*^e
- 5** Hawataabiki kama wana-damu wengine,^f
Wala hawateseki kama watu wengine.^g
- 6** Kwa hiyo, kiburi ni mkufu wao;^h
Ukatili huwafunika kama vazi.
- 7** Ufanisi wao* hufanya macho yao yanenepe;
Wamezidi mawazo ya moyo.

73:3 *Au "wanaojigamba." 73:4 *Au "Kitambi chao kimenenepa." 73:7 *Tnn., "Mafuta yao."

SURA YA 73

- a 2Nya 35:15
b Zb 84:11
Mt 5:8
c Zb 94:18
d Ayu 21:7
Yer 12:1
e Mhu 7:15
f Ayu 12:6
Ayu 21:7, 9
g Yer 12:1
h Ayu 21:14, 15

Safu ya 2

- a Zb 53:1
b 1Fa 21:7
c Zb 10:4, 11
Zb 94:3, 7
Eze 8:12
Sef 1:12
d Zb 37:35
e Zb 17:14
f Ayu 34:7, 9
Ayu 35:3
g Zb 34:19
h Ayu 7:17, 18

- 8** Wanadhikiki na kusema mambo maovu.^a
Kwa kiburi, wanatoa viti-sho vya kuwakandamiza wengine.^b
- 9** Wanaongea kana kwamba wako juu kama mbingu, Na ndimi zao hutamba duniani.
- 10** Kwa hiyo watu wake huwa-geukia,
Nao hunywa maji yao mengi.
- 11** Wanasema: "Mungu ana-juaje?"
Je, Aliye Juu Zaidi ana ujuzi kweli?"
- 12** Naam, hivyo ndivyo wa-livyo waovu, ambao sikuzote wanastarehe.^d
Wanaendelea kuongeza mali zao.^e
- 13** Kwa hakika nimeusafisha moyo wangu bure
Na kunawa mikono yangu katika ukosefu wa hatia.^f
- 14** Nami nilitaabika mchana kutwa;^g
Niliadhibiwa kila asubuhi.^h
- 15** Lakini kama ningesema mambo hayo,

- Ningewasaliti watu wako.*
- 16 Nilipojaribu kulielewa jambo hilo, Lilinitaabisha
- 17 Mpaka nilipoingia mahali patakatifu pa Mungu penye utukufu, Nami nikatambua wakati wao ujao.
- 18 Kwa hakika unawaweka kwenye ardhi yenye utelezi.^a Unawafanya waanguke katika uharibifu wao.^b
- 19 Jinsi wanavyoangamizwa kwa ghafla!^c Jinsi wanavyofikia kwa ghafla mwisho wao unaotisha!
- 20 Kama ndoto wakati wa kuamka, Ee Yehova, Utakapoinuka, utaitupilia mbali* sanamu yao.
- 21 Lakini moyo wangu ulikuwa mchungu,^d Na ndani kabisa* nilihisi maumivu makali.
- 22 Nilikuwa mpumbavu wala sikwa na ulewaji; Nilikuwa kama mnyama asiye na akili mbele zako.
- 23 Lakini sasa niko pamoja nawe sikuzote; Umeushika mkono wangu wa kulia.^e
- 24 Unaniongoza kwa ushauri wako,^f Na baadaye utaniongoza kwenye utukufu.^g
- 25 Ni nani niliye naye mbinguni? Isipokuwa wewe tu, sitamani chochote duniani.^h

73:15 *Tnn., "Ningekisaliti kizazi cha wana wako." 73:20 *Tnn., "utaidhara." 73:21 *Tnn., "katika figo zangu."

SURA YA 73

a Zb 35:6, 7
Yer 23:11, 12

b Zb 37:10, 20
Zb 55:23
Met 3:33

c Ayu 21:23
Zb 37:1, 2
Isa 30:13

d Zb 73:3

e Zb 16:8
Zb 63:8
Isa 41:10

f Zb 25:9
Zb 32:8
Zb 37:23
Zb 143:10
Met 3:6

g Zb 37:34

h Zb 42:2
Zb 84:2
Isa 26:9

Safu ya 2

a Zb 16:5
Omb 3:24

b Hes 15:39
Yak 4:4

c Zb 65:4
Yak 4:8

d Zb 118:17

SURA YA 74

e 1Nya 25:1
2Nya 35:15

f Omb 5:20

g Kum 29:19, 20
Zb 100:3

h Kum 9:29

i Kum 4:20
Kum 32:9

j Zb 48:2
Zb 132:13

k Da 9:17

l Zb 79:1

m Omb 2:7

- 26 Mwili wangu na moyo wangu unaweza kudhoo-fika, Lakini Mungu ni mwamba wa moyo wangu na fungu langu milele.^a
- 27 Kwa kweli, wale wanaojitenga mbali nawe wataangamia. Utamwangamiza* kila mtu anayekuacha kwa upotovu.^{#b}
- 28 Lakini kwa upande wangu, kumkaribia Mungu ni jambo jema kwangu.^c Nimemfanya Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova kuwa kimbilio langu, Ili nizitangaze kazi zako zote.^d

Maskili.* Wa Asafu.^e

- 74 Ee Mungu, kwa nini umetukataa milele?^f Kwa nini hasira yako inawaka* dhidi ya kundi la malisho yako?^g
- 2 Wakumbuke watu uliojipatia* zamani za kale,^h Kabila ulilokomboza liwe urithi wako.ⁱ Ukumbuke Mlima Sayuni, mahali unapokaa.^j
- 3 Zielekeze hatua zako kwenye magofu ya kudumu.^k Adui ameharibu kila kitu mahali patakatifu.^l
- 4 Maadui wako walinguruma ndani ya mahali pako pa mkutano.*^m Wameweka bendera zao wenyewe ziwe ishara humo.

73:27 *Tnn., "Utamnyamazisha." #Au "kukosa uaminifu." 74:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. 74:1 *Tnn., "inafuka moshi." 74:2 *Tnn., "Likumbuke kusanyiko lako ulilojipatia." 74:4 *Au "kusanyiko."

- 5 Walikuwa kama watu wanaotumia mashoka kufyeka msitu wenye miti mingi.
- 6 Walivunjavunja michongo yake yote^a kwa mashoka na fito za chuma.
- 7 Walichoma moto mahali pako patakatifu.^b Walichafua hema la ibada lenye jina lako, wakalia-ngusha chini.
- 8 Wao pamoja na uzao wao wamesema mioyoni mwao:
“Sehemu zote za Mungu za mikutano* zilizo nchini ni lazima ziteketezwe.”
- 9 Hatuoni ishara yoyote; Hakuna tena nabii yeyote, Na hakuna yeyote miongo-ni mwetu anayejua hali hii itaendelea hadi lini.
- 10 Ee Mungu, mpinzani ataendelea kudhihaki mpaka lini?^c
Je, adui ataendelea kudhiharau jina lako milele?^d
- 11 Kwa nini unauzuia mkono wako, mkono wako wa kuume?^e
Uchomoe kifuani mwako* na kuwangamiza.
- 12 Lakini Mungu ni Mfalme wangu tangu zamani za kale,
Yeye anayefanya matendo ya wokovu duniani.^f
- 13 Uliitibua bahari kwa nguvu zako;^g
Uliviponda vichwa vya wanyama wakubwa sana wa baharini.
- 14 Uliviponda vichwa vya Lewiathani*;

74:8 *Au “Sehemu zote ambazo Mungu anaabudiwa.” 74:11 *Au “Uchomoe kutoka katika makunjo ya vazi lako.” 74:14 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 74

a 1Fa 6:18, 35

b 2Fa 25:9
Isa 64:11c Zb 13:2
Zb 79:4

d Eze 36:23

e Zb 44:23
Isa 64:12
Omb 2:3f Kut 15:2
Isa 33:22g Kut 14:21
Ne 9:10, 11

Safu ya 2

a Isa 48:21

b Yos 3:13

c Mwa 1:3, 5
Zb 136:7, 8

d Mdo 17:26

e Mwa 8:22

f Isa 52:5

g Zb 12:5

h Ezr 3:11

i Zb 89:50, 51
Isa 52:5

Ukawapa watu wamle kama chakula chao, wale wanaokaa jangwani.

- 15 Ulipasua vijia kwa ajili ya chemchemi na vijito;^a
Ulikausha mito inayotiririka daima.^b
- 16 Mchana ni wako, na usiku pia.
Uliumba nuru* na jua.^c
- 17 Uliweka mipaka yote ya dunia;^d
Uliumba majira ya kianga-zi na majira ya baridi kali.^e
- 18 Kumbuka dhihaka za adui, Ee Yehova,
Jinsi taifa pumbavu lina-vyodharau jina lako.^f
- 19 Usiwape wanyama wa mwituni uhai wa* njiwa tetere wako.
Usiusahau milele uhai wa watu wako wanaoteseka.
- 20 Likumbuke lile agano,
Kwa maana sehemu za dunia zenye giza zimejaa makao ya ukatili.
- 21 Mtu aliyepondwa na asi-geuke na kwenda zake akiwa amekata tamaa;^g
Watu wa hali ya chini na maskini na walisifu jina lako.^h
- 22 Inuka, Ee Mungu, na utee kesi yako.
Kumbuka jinsi wapumbavu wanavyokudhihaki mchana kutwa.ⁱ
- 23 Usisahau mambo ambayo maadui wako wanasema.
Kelele za wale wanaokuasi zinapanda juu daima.

74:16 *Au “mwanga.” 74:19 *Au “nafsi ya.”

Kwa kiongozi. Umeptanishwa na muziki wa "Usiharibu." Wimbo wa Asafu.^a

- 75** Tunakushukuru, Ee Mungu, tunakushukuru;
Jina lako liko karibu,^b
Na watu wanatangaza kazi zako zinazostaajibisha.
- 2** Unasema: "Ninapoweka wakati hususa, Ninahukumu kwa haki.
- 3** Dunia na wakaaji wake wote walipoyeyushwa, Mimi ndiye niliyeziimari-sha nguzo zake." (*Sela*)
- 4** Ninawaambia wenye kuji-gamba, "Msijigambe," Na waovu, "Msikweze nguvu zenu."^{*}
- 5** Msikweze nguvu zenu^{*} juu sana Au kuongea kwa kiburi.
- 6** Kwa maana kukwezwwa hakutoki Mashariki wala magharibi wala kusini.
- 7** Kwa maana Mungu ni Mwamuzi.^c Humshusha huyu na kumkweza yule.^d
- 8** Kwa maana kuna kikombe mkononi mwa Yehova;^e Divai inatoa povu nayo imechanganywa kikamili. Hakika ataimwaga, Na waovu wote duniani watainywa, mpa-ka machicha yake."^f
- 9** Lakini mimi, nitalitangaza hilo milele; Nitamwambia sifa* Mungu wa Yakobo.
- 10** Kwa maana anasema: "Ni-

75:4, 5 * Tnn., "pembe yenu." 75:9 * Au "Nitampigia muziki."

SURA YA 75

a 2Nya 35:15

b Isa 30:27

c Zb 50:6
Zb 58:11d 1Sa 2:7
Da 2:21
Da 4:17
Lu 1:52

e Zb 11:5, 6

f Ayu 21:19, 20
Yer 25:15, 28
Yer 49:12
Ufu 14:9, 10
Ufu 16:19
Ufu 18:6

Safu ya 2

SURA YA 76

a 2Nya 35:15

b Zb 48:1, 3

c 2Nya 2:5

d Mwa 14:18

e Zb 74:2
Zb 132:13
Zb 135:21f 2Nya 32:21
Zb 46:9

g Lu 1:51

h Isa 31:8
Isa 37:36

i Nah 2:13

j Zb 89:7

k Yer 10:10
Nah 1:6

l 1Fa 8:49

m 2Nya 20:29
Zb 2:4, 5n Zb 147:6
Met 3:34
Sef 2:3

tazikata nguvu* zote za waovu."

Lakini nguvu* za waadilifu zitakwezwwa.

Kwa kiongozi; uimbwe kwa ala za nyuzi. Muziki wa Asafu.^a Wimbo.

76 Mungu anajulikana Yuda;^b

Jina lake ni kuu katika Israeli.^c

- 2** Banda lake liko Salemu,^d Na makao yake yako Sayuni.^e
- 3** Huko aliivunja mishale inayowaka ya upinde, Ngao na upanga na silaha za vita.^f (*Sela*)
- 4** Unang'aa kwa uangavu;^{*} Una fahari kuliko milima ya mawindo.
- 5** Wenye moyo jasiri wameporwa.^g Wamelala usingizi; Mashujaa wote hawakuwa na uwezo.^h
- 6** Kwa sababu ya kemeo lako, Ee Mungu wa Yakobo, Mwendeshaji wa gari na farasi wote wamelala usingizi mzito.ⁱ
- 7** Ni wewe peke yako una-yeogopesha.^j Na ni nani anayeweza kustahimili hasira yako kali?^k
- 8** Kutoka mbinguni ulitangaza hukumu;^l Dunia iliogopa na kunyamaza^m
- 9** Mungu alipoinuka ili kutekeleza hukumu, Ili kuwaokoa wapole wote walio duniani.ⁿ (*Sela*)
- 10** Kwa maana ghadhabu ya

75:10 * Tnn., "pembe." 76:4 * Au "Ume-funikwa na nuru."

mwanadamu itakuletea sifa.^a

Nawe utajipamba kwa mabaki ya ghadhabu yao.

- 11** Wekeni nadhiri zenu kwa Yehova Mungu wenu na kuzitimiza,^b

Wote wanaomzunguka na walete zawadi yao kwa woga.^c

- 12** Atakinyenyekeza kibiri cha* viongozi;

Yeye huwaogopesha wafalme wa dunia.

Kwa kiongozi; mtindo wa Yeduthuni.* Muziki wa Asafu.^d

- 77** Kwa sauti yangu nitamlilia Mungu; Nitamlilia Mungu kwa sauti kubwa, naye atanisikia.^e

- 2** Katika siku ya taabu yangu ninamtafuta Yehova.^f

Usiku ninamnyooshea mikono yangu bila kuacha.*

Siwezi[#] kufarijiwa.

- 3** Ninapomkumbuka Mungu, ninalia kwa maumivu;^g

Ninataabika na nguvu zangu zinaniishia.*^h (*Sela*)

- 4** Unazishika kope zangu ili nisifumbe macho; Nimefadhaika, nami siwezi kuongea.

- 5** Mawazo yangu yanarudi katika siku za zamani za kale,ⁱ

Miaka mingi iliyopita.

- 6** Wakati wa usiku ninakuimbuka wimbo wangu,*^j

76:12 *Tnn., "Atainyenyekeza roho ya."
77:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.
77:2 *Tnn., "bila kufa ganzi." #Au "Nafsi yangu haiwezi." 77:3 *Tnn., "roho yangu inazimia." 77:6 *Au "muziki wangu wa nyuzi."

SURA YA 76

a Met 16:4
Da 3:19, 28

b Hes 30:2

c 2Nya 32:23
Zb 89:7

SURA YA 77

d 2Nya 35:15

e Zb 34:6
Met 15:29

f Zb 18:6
Zb 50:15

g Zb 42:5

h Zb 143:4

i Zb 143:5
Isa 51:9

j Zb 42:8

Safu ya 2

a Zb 77:12

b Zb 74:1

c Zb 79:5

d Isa 49:14
Isa 63:15

e Zb 31:22

f 1Nya 16:9
Zb 143:5

g Kut 15:11
Zb 89:8

h Zb 72:18
Ufu 15:3

i Kut 9:16
Isa 52:10
Da 3:29
Da 6:26, 27

j Kut 6:6
Kum 9:29

Ninatafakari moyoni mwangu;^a

Ninatafuta* kwa bidii.

- 7** Je, Yehova atatutupa mbali milele?^b

Je, hatatuonyesha tena kamwe kibali chake?^c

- 8** Je, upendo wake mshikamanifu utakoma milele?

Je, ahadi yake itakosa kutimia katika vizazi vyote?

- 9** Je, Mungu amesahau kuo-nyesha kibali chake,^d

Au je, hasira yake imekomesha rehema yake? (*Sela*)

- 10** Je, ni lazima niendeleo kusema: "Hili ndilo linalonitaabisha.*^e

Aliye Juu Zaidi amebadili msimamo wake kutuelekea?"[#]

- 11** Nitazikumbuka kazi za Yah;

Nitayakumbuka matendo yako yanayostaajibisha ya zamani za kale.

- 12** Nitautafakari utendaji wako wote Na kutafakari shughuli zako.^f

- 13** Ee Mungu, njia zako ni takatifu.

Ee Mungu, ni mungu gani aliye mkuu kama wewe?^g

- 14** Wewe ndiye Mungu wa kweli, unayetenda mambo yanayostaajibisha.^h

Umeyafunulia mataifa nguvu zako.ⁱ

- 15** Kwa nguvu zako* ume-
waokoa[#] watu wako,^j

77:6 *Tnn., "Roho yangu inatafuta."
77:10 *Au "linalonichoma." #Tnn., "amebadili mkono wake wa kuume dhidi yetu." 77:15 *Tnn., "mkono wako." #Tnn., "umewakomboa."

Wana wa Yakobo na wa Yosefu. (*Sela*)

16 Maji yalikuona, Ee Mungu, Maji yalikuona yakavurugika.^a

Na vilindi vya maji vikati-buka.

17 Mawingu yakamwaga maji.

Anga lenye mawingu likanguruma,

Na mishale yako ikaruka huku na kule.^b

18 Sauti ya mngurumo^c wako ilikuwa kama magurudumu ya gari la vita;

Mimweko ya radi ilianguza dunia inayokaliwa;^{*d}

Dunia ilitikisika na kutetemeka.^e

19 Njia yako ilipita baharini,^f Kijia chako kilipita katika maji mengi;

Lakini nyayo zako hazingeweza kuonekana.

20 Uliwaongoza watu wako kama kundi la kondoo,^g Chini ya uangalizi* wa Musa na Haruni.^h

Maskili.* Wa Asafu.ⁱ

78 Sikilizeni sheria* yangu, enyi watu wangu;

Tegeni sikio lenu kwa maneno ya kinywa changu.

2 Nitakifungua kinywa changu kwa methali.

Nitafumbua mafumbo ya zamani za kale.^j

3 Mambo ambayo tumesikia na tunayojua, Ambayo baba zetu wame-tusimulia,^k

4 Hatutawaficha wana wao;

77:18 *Au "ardhi inayozaa." **77:20** *Tnn., "Kwa mkono." **78:Uta** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **78:1** *Au "mafundisho."

SURA YA 77

a Kut 14:21
Yos 3:16
Zb 114:1-3

b 2Sa 22:15
Zb 144:6

c Zb 29:3

d Zb 97:4

e Kut 19:18
2Sa 22:8

f Ne 9:10, 11
Hab 3:15

g Kut 13:21
Zb 78:52

h Isa 63:11
Mdo 7:35, 36

SURA YA 78

i 1Nya 25:1

j Met 1:5, 6
Mt 13:34, 35

k Kut 13:8
Zb 44:1

Safu ya 2

a Kum 4:9
Kum 6:6, 7
Kum 6:21
Kum 11:18, 19
Yos 4:6, 7

b Isa 63:7

c Zb 98:1

d Mwa 18:19
Kum 6:6, 7

e Zb 71:17, 18
Zb 102:18

f Kum 4:10

g Kum 4:9
Zb 103:2

h Kum 5:29

i Kut 32:9
Kum 1:43
Kum 31:27
2Fa 17:13, 14
Eze 20:18
Mdo 7:51

j Zb 81:11, 12
Yer 7:24-26

k Kum 31:16

l 2Nya 13:8, 9
Ne 9:26

m Kum 32:18
2Nya 13:12
Yer 2:32

n Zb 106:21, 22

Tutakisimulia kizazi kijacho mambo hayo^a

Matendo ya Yehova yanayostahili sifa na nguvu zake,^b

Mambo yanayostaajibisha aliyotenda.^c

5 Alianzisha kikumbusho katika Yakobo

Na kuweka sheria katika Israeli;

Aliwaamuru mababu zetu Wawajulishe watoto wao mambo hayo,^d

6 Ili kizazi kijacho, Watoto ambao hawajazaliwa, wayajue.^e

Kisha wao watawasimulia watoto wao.^f

7 Halafu watoto hao watamtumaini Mungu.

Hawatasahau kazi za Mungu^g

Lakini watashika amri zake.^h

8 Kisha hawatakuwa kama mababu zao,

Kizazi chenye ukaidi na uasi,ⁱ

Kizazi kilichokuwa na moyo unaoyumba-yumba^{*j}

Na ambacho hakikuwa na roho ya uaminifu kwa Mungu.

9 Waefraimu walijihami kwa upinde,

Lakini walikimbia siku ya vita.

10 Hawakushika agano la Mungu^k

Nao walikataa kutembea katika sheria yake.^l

11 Walisahau pia mambo aliyotenda,^m

Kazi zake zinazostaajibisha alizowaonyesha.ⁿ

78:8 *Tnn., "ambao haujatayarishwa."

- 12** Alifanya maajabu mbele ya mababu zao,^a Katika nchi ya Misri, eneo la Soani.^b
- 13** Aliipasua bahari ili kuwaruhusu wavuke, Naye akayafanya maji yasimame juu kama bwawa.*^c
- 14** Aliwaongoza kwa wingu wakati wa mchana Na usiku kucha kwa mwangaza wa moto.^d
- 15** Aliipasua miamba nyikani, Akawanyweshwa maji ya kutosha kana kwamba yanatoka vilindini.^e
- 16** Alivitoa vijito kutoka kwenye jabali Na kufanya maji yatiririke chini kama mito.^f
- 17** Lakini waliendelea kumtendea dhambi Kwa kumwasi jangwani yule Aliye Juu Zaidi;^g
- 18** Walimjaribu* Mungu moyoni mwao^h Walidai wapewe chakula walichotamani.[#]
- 19** Kwa hiyo wakalalamika kumhusu Mungu, Wakisema: "Je, Mungu anaweza kuandaa meza nyikani?"ⁱ
- 20** Tazama! Aliupiga mwamba Hivi kwamba maji yakatiririka na vijito vikafurika.^j "Je, anaweza pia kutupatia mkate, Au je, anaweza kuwapa watu wake nyama?"^k
- 21** Yehova alipowasikia, alikasirika sana!^l

78:13 *Au "ukuta." 78:18 *Tnn., "Walimtahini." #Au "chakula kwa ajili ya nafsi yao."

SURA YA 78

a Kum 4:34
Ne 9:10

b Hes 13:22

c Kut 14:21, 22
Kut 15:8

d Kut 13:21
Kut 14:20, 24

e Kut 17:6
Hes 20:11
Zb 105:41
Isa 48:21
1Ko 10:4

f Kum 8:14, 15

g Kum 9:21, 22
Zb 95:8
Ebr 3:16

h Zb 106:14

i Kut 16:8

j Kut 17:6

k Kut 16:3

l Hes 11:10

Safu ya 2

a Ebr 12:29

b Hes 11:1

c Zb 106:24
Ebr 3:10
Yud 5

d Kut 16:14, 35
Kut 16:31, 32
Hes 11:7
Kum 8:3
Yoh 6:31
1Ko 10:2, 3

e Zb 103:20

f Kut 16:12

g Hes 11:31-34

h Hes 11:19, 20

i Hes 11:10

j Hes 11:34

- Moto^a ukawaka dhidi ya Yakobo, Na hasira yake ikawaka dhidi ya Israeli^b
- 22** Kwa sababu hawakudhihirisha imani katika Mungu;^c Hawakuutumaini uwezo wake wa kuwaokoa.
- 23** Basi akaliamuru anga lililo juu lenye mawingu, Naye akaifungua milango ya mbingu.
- 24** Akaendelea kuwanyeshea mana ili wale; Akawapa nafaka ya mbinguni.^d
- 25** Wanadamu wakala mkate wa wenye nguvu;^{*e} Aliwapa mkate wa kutosha wa kuwashibisha.^f
- 26** Aliuvumisha upepo wa mashariki mbinguni Na kwa nguvu zake akayafanya upepo wa kusini uvume.^g
- 27** Naye akawanyeshea nyama kama mavumbi, Ndege kama mchanga kwenye ufuo wa bahari.
- 28** Aliwaangusha katikati ya kambi yake, Pande zote kuzunguka mahema yake.
- 29** Nao wakala na kujilazimisha kula zaidi; Aliwapa walichotamani.^h
- 30** Lakini kabla hawajatosheleza kikamili tamaa yao, Chakula kilipokuwa kingali kinywani mwao,
- 31** Ghadhabu ya Mungu ikawaka dhidi yao.ⁱ Akawaua wanaume wenye nguvu zaidi;^j Aliwaangamiza wanaume vijana wa Israeli.

78:25 *Au "wa malaika."

- 32** Licha ya hayo walizidi kutenda dhambi^a
Nao hawakudhihirisha imani katika kazi zake zinazostaajabisha.^b
- 33** Basi akazikatisha siku zao kana kwamba ni pumzi tu,^c
Na miaka yao kwa matukio ya ghafla yenye kutisha.
- 34** Lakini kila mara ali-powaua baadhi yao, waliosalia walimtafuta;^d
Walirudi na kumtafuta Mungu,
- 35** Wakikumbuka kwamba Mungu alikuwa Mwamba wao^e
Na kwamba Mungu Aliye Juu Zaidi alikuwa Mko-mbozi* wao.^f
- 36** Lakini walijaribu kumda-nganya kwa kinywa chao
Na kumwambia uwongo kwa ulimi wao.
- 37** Moyo wao haukuwa imara kumwelekea;^g
Nao hawakuwa waaminifu kwa agano lake.^h
- 38** Lakini alikuwa mwenye rehema;ⁱ
Alikuwa akiwasamehe* kosa lao, naye hakuwa-ngamiza.^j
Mara nyingi aliizuia hasira yake^k
Badala ya kuichochea ghadhabu yake yote.
- 39** Kwa maana alikumbuka kwamba walikuwa nyama tu,^l
Upepo upitao ambao hau-rudi.*
- 40** Jinsi walivyomwasi mara nyingi nyikani^m

78:35 *Au "Mlipiza-Kisasi." **78:38** *Tnn., "akifunika." **78:39** *Au labda, "Kwamba roho inaenda nayo hairudi."

SURA YA 78

a Hes 14:2-4
Hes 25:3
1Ko 10:8-10

b Kut 16:15
Kum 8:14, 15

c Hes 14:29, 35
Kum 2:14

d Hes 21:7
Amu 4:3

e Kum 32:4

f Kut 6:6

g Zb 95:10
Ebr 3:10

h Kum 31:20
Yer 31:32

i Kut 34:6
Hes 14:18
Ne 9:31

j Hes 14:19, 20
Yer 30:11
Omb 3:22

k Ne 9:27
Isa 48:9
Eze 20:9

l Zb 103:14

m Hes 14:11

Safu ya 2

a Isa 63:10
Efe 4:30
Ebr 3:16

b Hes 14:22
Kum 6:16
Zb 95:8, 9

c Kut 14:30

d Kum 4:34
Ne 9:10
Zb 105:27-36

e Kut 7:19

f Kut 8:24

g Kut 8:6

h Kut 10:14, 15

i Kut 9:23

j Kut 9:25

Na kumtia uchungu jangwani!^a

- 41** Walimjaribu Mungu tena na tena,^b
Nao wakamhuzunisha* Mtakatifu wa Israeli.
- 42** Hawakuzikumbuka nguvu zake,^{*}
Siku ambayo aliwaokoa[#] kutoka kwa adui,^c
- 43** Jinsi alivyoonyesha ishara zake kule Misri^d
Na miujiza yake katika eneo la Soani,
- 44** Na jinsi alivyobadili mife-reji ya Nile kuwa damu^e
Hivi kwamba hawangewe-za kunywa maji kutoka katika vijito vyake.
- 45** Alituma makundi ya nzi ili yawale^f
Na vyura ili kuwaanga-miza.^g
- 46** Mazao yao aliwapa parare wanaokula sana,
Matunda ya kazi yao ngu-mu akayapa makundi ya nzige.^h
- 47** Aliharibu mizabibu yao kwa mvua ya maweⁱ
Na mikuyu yao kwa mawe ya mvua.
- 48** Aliwaua kwa mvua ya mawe wanyama wao wa kubeba mizigo^j
Na mifugo yao kwa umeme wa radi.*
- 49** Aliwamwagia hasira yake inayowaka,
Hasira kali na ghadhabu na taabu,
Makundi ya malaika yana-yoleta msiba.

78:41 *Au "wakamtia uchungu." **78:42** *Tnn., "Hawakuukumbuka mkono wake." **78:43** *Tnn., "aliwakomboa." **78:48** *Au labda, "homa kali."

- 50** Alitayarisha njia kwa ajili ya hasira yake.
Hakuwalinda wasife;*
Naye aliwaua kwa ugonjwa hatari.
- 51** Mwishowe aliwaangamiza wazaliwa wote wa kwanza wa Misri,^a
Mwanzo wa nguvu zao za uzazi katika mahema ya Hamu.
- 52** Kisha akawatoa nje watu wake kama kundi la kondoo^b
Na kuwaongoza nyikani kama kundi la mifugo.
- 53** Aliwaongoza kwa usalama,
Nao hawakuogopa;^c
Bahari ili wafunika maadui wao.^d
- 54** Naye akawaleta katika eneo lake takatifu,^e
Eneo hili lenye milima ambalo mkono wake wa kuume ulilitwaa.^f
- 55** Aliyafukuza mataifa kuto-ka mbele yao;^g
Akawagawia urithi kwa kamba ya kupimia;^h
Aliyafanya makabila ya Israeli yakae katika makao yao.ⁱ
- 56** Lakini waliendelea kumjaribu* Mungu Aliye Juu Zaidi, na kumwasi;^j
Hawakusikiliza vikumbusho vyake.^k
- 57** Pia walipotoka na kutenda kwa hila kama mababu zao.^l
Hawakutegemeka kama upinde uliolegea usivyo-tegemeka.^m
- 58** Waliendelea kumkasirisha kwa mahali pao pa juu,ⁿ

78:50 *Au "Hakulinda nafsi zao zisife."
78:56 *Au "kumtahini."

SURA YA 78

a Kut 12:29
Zb 105:36

b Zb 77:20
Zb 105:37

c Kut 14:20
Ebr 11:29

d Kut 14:27
Kut 15:10

e Kut 15:17

f Zb 44:3

g Yos 24:12
Zb 44:2

h Yos 13:7

i Ne 9:24, 25

j Kum 31:16
Kum 32:15

Amu 2:11
2Sa 20:1
Ne 9:26

k 2Fa 17:15
Yer 44:23

l Kum 9:7
Amu 3:6

m Ho 7:16

n Kum 12:2
Amu 2:2
Eze 20:28

Safu ya 2

a Amu 2:12
1Sa 7:3

b Amu 2:20

c Yos 18:1
1Sa 4:11

d Yer 7:12

e 1Sa 4:21
1Sa 5:1

f 1Sa 4:2, 10

g 1Sa 2:33, 34
1Sa 4:11

h 1Sa 4:19

i Zb 44:23

j Isa 42:13

k 1Sa 5:6

l Mwa 49:10

m Zb 87:2
Zb 132:13
Zb 135:21

Nao wakachochea hasira yake kali* kwa sanamu zao za kuchongwa.^a

- 59** Mungu alisikia na kuwaka hasira,^b
Kwa hiyo akaikataa kabisa Israeli.
- 60** Mwishowe akaliacha hema la ibada lililo Shilo,^c
Hema alimokaa miongoni mwa wanadamu.^d
- 61** Aliacha ishara ya nguvu zake ipelekwe utekwani;
Fahari yake itiwe mikononi mwa adui.^e
- 62** Aliwatoa watu wake wauawe kwa upanga^f
Naye akaukasirikia vikali urithi wake.
- 63** Moto uliwateketeza kabisa vijana wake wa kiume,
Na mabikira wake hawakuimbiwa nyimbo za harusi.*
- 64** Makuhani wake waliuawa kwa upanga,^g
Na wajane wao hawakulia.^h
- 65** Kisha Yehova akaamka kana kwamba anatoka usingizini,ⁱ
Kama mwanamume hodari^j aamkavyo baada ya divai kumtoka.
- 66** Naye akawakimbiza maadui wake;^k
Akawatia aibu ya kudumu.
- 67** Alilikataa hema la Yosefu; Hakulichagua kabila la Efraimu.
- 68** Lakini alichagua kabila la Yuda,^l
Mlima Sayuni, anaoupe-nda.^m
- 69** Alipafanya mahali pake patakatifu pawe mahali

78:58 *Au "wivu wake." 78:63 *Tnn., "hawakusifiwa."

- pa kudumu kama mbingu,^{*a}
Kama dunia ambayo ameiimarisha milele.^b
- 70** Alimchagua Daudi^c mtumishi wake
Na kumtoa katika mazizi ya kondoo,^d
- 71** Alimwondoa katika kazi ya kuchunga kondoo wa-naonyonyesha;
Akamfanya kuwa mchungaji wa Yakobo, watu wake.^e
Na wa Israeli, urithi wake.^f
- 72** Aliwachunga kwa utimili-fu wa moyo,^g
Na kwa mikono stadi ali-waongoza.^h
Muziki wa Asafu.ⁱ
- 79** Ee Mungu, mataifa ya-mevamia urithi wako;^j
Yamelichafua hekalu lako takatifu;^k
Yamebadili Yerusalemu kuwa rundo la magofu.^l
- 2** Wamewapa ndege wa angani maiti za watumishi wako kuwa chakula chao
Na miili ya washikamanifu wako wamewapa wanyama wa mwituni wa dunia.^m
- 3** Wamewaga damu yao kama maji kotekote Yerusalemu,
Na hakuna aliyebaki wa kuwazika.ⁿ
- 4** Tumekuwa kitu cha kushutumwiwa na majirani wetu;^o
Wale wanaotuzunguka wanatudhihaki na kutufanyia mzaha.

78:69 *Tnn., "Alipajenga mahali pake patakatifu kama vilele."

SURA YA 78

- a Zb 76:2
b Zb 104:5
Zb 119:90
Mhu 1:4
c 1Sa 16:12, 13
d 1Sa 17:15
e 2Sa 7:8
f 2Sa 6:21
g 2Sa 8:15
1Fa 3:6
1Fa 9:4
1Fa 15:5
h 1Sa 18:14

SURA YA 79

- i 1Nya 25:1
j Kut 15:17
k 2Fa 24:12, 13
Zb 74:3, 7
Omb 1:10
l 2Fa 25:9, 10
2Nya 36:17-19
Yer 52:13
m Yer 7:33
Yer 15:3
Yer 34:20
n Yer 14:16
Yer 16:4
o Kum 28:37
Eze 36:4

Safu ya 2

- a Zb 74:1
Zb 85:5
Isa 64:9
b Sef 1:18
c Yer 10:25
d 2Nya 36:20, 21
e Ne 9:34
f Zb 69:17
Omb 3:22
g 1Nya 16:35
h Yos 7:9
1Sa 12:22
2Nya 14:11
Zb 115:1, 2
Isa 48:9
Yer 14:7
i Yoe 2:17
j Yer 51:35
Eze 36:23
k Kut 2:23
Isa 42:6, 7
l Zb 102:19, 20
m Yer 12:14

- 5** Ee Yehova, utaendelea kuwaka hasira mpaka lini? Milele?^a
Ghadhabu yako itaendelea kuwaka kama moto mpaka lini?^b
- 6** Yamwagie ghadhabu yako mataifa ambayo hayakujui
Na falme ambazo haziliitii jina lako.^c
- 7** Kwa maana wamemnyafua Yakobo
Nao wameifanya nchi yake ukiwa.^d
- 8** Usitufanye tuwajibike kwa sababu ya makosa ya mababu zetu.^e
Tuonyeshe haraka rehema yako,^f
Kwa maana tumeshushwa chini sana.
- 9** Tusaidie, Ee Mungu wa wokovu wetu,^g
Kwa ajili ya jina lako tukufu;
Tuokoe na kutusamehe* dhambi zetu kwa ajili ya jina lako.^h
- 10** Kwa nini mataifa yaseme: "Mungu wao yuko wapi?"ⁱ
Na ijulikane miongoni mwa mataifa mbele ya macho yetu
Kwamba damu iliyomwagwa ya watumishi wako imelipiziwa kisasi.^j
- 11** Na usikie kilio cha maumivu cha mfungwa.^k
Tumia nguvu zako kuu* kuwahifadhi* wale waliohukumiwa kifo.^{Δl}
- 12** Walipize majirani wetu mara saba^m

79:9 *Tnn., "ufunike." 79:11 *Tnn., "mkono wako." # Au labda, "kuwaweka huru." Δ Tnn., "wana wa kifo."

Kwa sababu ya shutuma walizotoa dhidi yako, Ee Yehova.^a

- 13** Kisha sisi, watu wako na kondoo wa malisho yako,^b
Tutakushukuru milele;
Nasi tutatangaza sifa yako kizazi mpaka kizazi.^c

Kwa kiongozi; umepatanishwa na mtindo wa "Mayungiyungi." Kikumbusho. Muziki wa Asafu.^d

- 80** Ee Mchungaji wa Israeli, sikiliza,

Wewe unayemwongoza Yosefu kama kundi la kondoo.^e

Wewe unayeketi kwenye kiti cha ufalme juu ya* makerubi,^f

Angaza.[#]

- 2** Mbele ya Efraimu na Benjamini na Manase, Chochea nguvu zako;^g
Njoo utuokoe.^h
- 3** Ee Mungu, turudishe;ⁱ
Uso wako na utuangazie, ili tuokolewe.^j
- 4** Yehova Mungu wa majeshi, utaendelea mpaka lini kuwa na hasira kali kuelekea* sala ya watu wako?^k
- 5** Unawalisha machozi kama mkate,
Nawe unawanyesha machozi kupita kiasi.
- 6** Unawaruhusu majirani wetu wagombane kwa sababu yetu;
Maadui wetu wanaendelea kutudhihaki wapendavyo.^l
- 7** Ee Mungu wa majeshi, turudishe;

80:1 *Au labda, "katikati ya." #Au "Funa uangavu wako." **80:4** *Tnn., "kuwaka hasira dhidi ya."

SURA YA 79

a Zb 74:18

b Zb 74:1
Zb 95:7
Zb 100:3

c Zb 145:4
Isa 43:21

SURA YA 80

d 1Nya 25:1

e Zb 77:20
Isa 40:11
Yer 31:10
Eze 34:12
1Pe 2:25

f Kut 25:20, 22
1Sa 4:4

g Isa 42:13

h Isa 25:9

i Zb 85:4
Omb 5:21

j Hes 6:25
Zb 67:1, 2

k Zb 74:1
Zb 85:5
Omb 3:44

l Zb 44:13
Zb 79:4

Safu ya 2

a Zb 80:3, 19

b Isa 5:7

c Zb 44:2
Zb 78:55
Yer 2:21

d Kut 23:28, 30
Yos 24:12, 13
1Fa 4:25

e Mwa 15:18
Kut 23:31
1Fa 4:21
Zb 72:8

f Isa 5:5

g Nah 2:2

h 2Fa 18:9
2Fa 24:1
2Fa 25:1
2Nya 32:1
Yer 39:1

i Isa 63:15

j Isa 5:7
Yer 2:21

k Kut 4:22
Isa 49:5

l Zb 79:5
Yer 52:12, 13

Uso wako na utuangazie, ili tuokolewe.^a

- 8** Uliufanya mzabibu^b uondoke Misri.
Uliyafukuza mataifa na kuupanda.^c
- 9** Ulitayarisha nafasi kwa ajili yake,
Nao ukatia mizizi na kujaa nchini.^d
- 10** Milima ilifunikwa kwa kivuli chake,
Na mierzizi ya Mungu kwa matawi yake.
- 11** Matawi yake yalienea mpaka baharini,
Na machipukizi yake mpaka kwenye Mto Efrati.^e
- 12** Kwa nini umebomoa kuta za mawe za shamba la mzabibu huo,^f
Hivi kwamba wote wanaopita karibu nao wanachuma matunda yake?^g
- 13** Nguruwe wa mwituni wanauhharibu,
Na wanyama wa porini wanaula.^h
- 14** Ee Mungu wa majeshi, rudi tafadhali.
Tazama chini kutoka mbinguni uone!
Utunze mzabibu huu,ⁱ
- 15** Shina* ambalo mkono wako wa kuume ume-panda,^j
Na umtazame mwana ambaye umemtia nguvu[#] kwa ajili yako mwenyewe.^k
- 16** Umechomwa moto,^l ume-katwa.
Wanaangamia kwa kemeo lako.*

80:15 *Au "Shina kuu la mzabibu." #Au "ulitazame tawi ambalo umelitia nguvu." **80:16** *Tnn., "kwa kemeo la uso wako."

17 Mkono wako na umtegemeze mwanamume aliye kwenye mkono wako wa kuume,

Mwana wa binadamu uliyemtia nguvu kwa ajili yako mwenyewe.^a

18 Kisha hatutageuka kutoka kwako.

Tuhifadhi hai, ili tuliitie jina lako.

19 Ee Yehova Mungu wa majeshi, turudishe; Uso wako na utungazie, ili tuokolewe.^b

Kwa kiongozi; juu ya Gitithi.*
Wa Asafu.^c

81 Mshangilieni Mungu kwa sauti, nguvu zetu.^d

Mpazieni sauti kwa ushindi Mungu wa Yakobo.

2 Anzisheni muziki na kuchukua tari, Kinubi chenye sauti tamu pamoja na kinanda.

3 Pigeni pembe wakati wa mwezi mpya,^e Wakati wa mwezi mpevu, kwa ajili ya siku ya she-rehe yetu.^f

4 Kwa maana ni agizo kwa Israeli, Sheria ya Mungu wa Yakobo.^g

5 Aliiweka ili iwe kikumbusho kwa Yosefu^h Alipoenda* kuishambulia nchi ya Misri.ⁱ Nilisikia sauti[#] ambayo sikuitambua:

6 "Niliuinua mzigo kutoka begani mwake;^j Mikono yake iliwekwa huru kutoka kwenye kikapu.

81:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.
81:5 *Yaani, Mungu. #Au "lugha."

SURA YA 80

a Zb 89:20, 21

b Zb 80:7

SURA YA 81

c 1Nya 25:1

d Zb 28:8

e Hes 29:1

f Kut 23:16
Hes 10:10

g Law 23:23, 24

h Kut 12:14

i Kut 12:12

j Kut 1:13, 14
Kut 6:6

Safu ya 2

a Kut 14:10, 13
Zb 91:15

b Kut 19:16, 19

c Kut 17:6, 7

d Kut 15:26

e Kut 20:2-5
Kum 6:13, 14

f Kum 5:6

g Kum 32:13, 14

h Kut 32:1
Kum 32:15

i Yer 7:23, 24
Yer 11:7, 8
Mik 6:16

j Kum 32:29

k Kum 5:29
Isa 48:17, 18

l Hes 14:9

7 Katika taabu uliita, nani nikakuokoa;^a Nilikujibu kutoka katika wingu lenye ngurumo.*^b Nilikujaribu katika maji ya Meriba.^{#c} (Sela)

8 Sikieni, watu wangu, nani nitatoa ushahidi dhidi yenu. Ee Israeli, laiti ungenisikiliza.^d

9 Hakutakuwa na mungu yeyote wa kigeni miongoni mwenu; Nanyi hamtamwinamia mungu wa kigeni.^e

10 Mimi, Yehova, ni Mungu wako, Niliyekutoa nchini Misri.^f Fungua wazi kinywa chako, nani nitakijaza.^g

11 Lakini watu wangu hawa-kuisikiliza sauti yangu; Israeli hakujitiisha kwa-ngu.^h

12 Kwa hiyo nikawaacha wafuate mioyo yao mikaidi; Walitenda mambo waliyofikiri yanafaa.*ⁱ

13 Laiti watu wangu wangenisikiliza,^j Laiti Israeli angetembea katika njia zangu!^k

14 Ningewatiisha haraka maadui wao; Ningeugeza mkono wangu dhidi ya wapinzani wao.^l

15 Wale wanaomchukia Yehova watajikunyata mbele zake, Na mwisho* wao utakuwa wa milele.

81:7 *Tnn., "katika mahali palipofichika pa ngurumo." #Maana yake "Kugombana." 81:12 *Tnn., "Walitembea katika mashauri yao." 81:15 *Tnn., "wakati."

16 Lakini atakulisha* ngano bora kabisa^{#a}
Na kukushibisha kwa asali kutoka mwambani.”^b

Muziki wa Asafu.^c

82 Mungu anachukua mahali pake katika kusanyiko la Mungu;^d
Anahukumu katikati ya miungu.*^e

2 “Mtaendelea mpaka lini kuhukumu bila haki^f
Na kuwapelelea waovu?^g (Sela)

3 Mteteeni* mtu wa hali ya chini na yatima.^h
Mtendeeni kwa haki mtu asiye na uwezo na maskini.ⁱ

4 Mwokoeni mtu wa hali ya chini na maskini;
Waokoeni kutoka mkononi mwa mwovu.”

5 Hawajui wala hawaelewi;^j
Wanatembea huku na huku gizani;
Misingi yote ya dunia inatikiwa.^k

6 “Nimesema, ‘Ninyi ni miungu,*^l

Ninyi nyote ni wana wa Aliye Juu Zaidi.

7 Lakini mtakufa kama wanadamu wanavyokufa;^m
Nanyi mtaanguka kama mkuu mwingine yeyote anavyoanguka!”ⁿ

8 Inuka, Ee Mungu, uihukumu dunia,^o
Kwa maana mataifa yote ni yako.

81:16 *Tnn., “atamlisha,” yaani, watu wa Mungu. [#]Tnn., “mafuta ya ngano.” 82:1 *Au “walio kama miungu.” 82:3 *Au “Hukumuni kwa ajili ya.” 82:6 *Au “ni kama miungu.”

SURA YA 81

a Zb 147:14

b Kum 32:13, 14

SURA YA 82

c 1Nya 25:1

d 2Nya 19:6

e Kut 18:21, 22
Zb 82:6
Yoh 10:34, 35

f Law 19:15
Mhu 5:8

g Kum 1:16, 17
2Nya 19:7
Met 18:5

h Kum 24:17

i Yer 22:3

j Mik 3:1

k Zb 11:3
Met 29:4

l Yoh 10:34, 35
1Ko 8:5

m Zb 49:12

n Zb 146:3, 4

o Zb 96:13

Safu ya 2

SURA YA 83

a 2Nya 20:14

b Zb 28:1

c Zb 2:1, 2

d Kut 1:8-10
2Nya 20:1
Est 3:6

e 2Sa 10:6
Isa 7:2, 5

f 2Nya 20:1, 10

g 1Nya 5:10

h Yer 49:2

i Kut 15:14
Zb 60:8

j Amo 1:9

k 2Fa 17:5

l Mwa 19:36-38
Kum 2:9

m Amu 8:10, 12

n Amu 4:2, 7, 15

o Yos 17:11

Wimbo. Muziki wa Asafu.^a
83 Ee Mungu, usinya maze;^b
Usikae kimya wala kutulia, Ee Mungu.

2 Kwa maana, tazama! Maudui wako wanafanya fujo;^c

Wale wanaokuchukia wanatenda kwa kiburi.*

3 Kwa hila wanapanga njama kwa siri dhidi ya watu wako;

Wanapanga njama dhidi ya watu wako unaowathamini.*

4 Wanasema: “Njoooni, acheni tuwaangamize wakiwa taifa,^d

Ili jina la Israeli lisikumbu-kwe tena kamwe.”

5 Kwa umoja wanatunga mbinu;*
Wameungana[#] dhidi yako^e—

6 Mahema ya Edomu na Waishmaeli, Moabu^f na Wahagri,^g

7 Gebali na Amoni^h na Amaleki,
Ufilistiⁱ pamoja na wakaaji wa Tiro.^j

8 Pia Ashuru^k imejiunga nao;

Wanawaunga mkono* wana wa Loti.^l (Sela)

9 Watendee kama ulivyoitendea Midiani,^m

Kama ulivyomtendea Sissera na Yabini kwenye kijito cha* Kishoni.ⁿ

10 Waliangamizwa kule En-dori;^o

83:2 *Au “wanainua vichwa vyao.” 83:3 *Tnn., “waliofichwa.” 83:5 *Tnn., “Wanashauriana kwa moyo mmoja.” *Au “Wamefanya agano.” 83:8 *Tnn., “Wamekuwa mkono kwa.” 83:9 *Au “korongo la.”

Wakawa mbolea juu ya ardhi.

- 11 Wafanye viongozi wao wawe kama Orebu na Zeebu^a

Na wakuu* wao kama Zeba na Zalmuna,^b

- 12 Kwa maana walisema: “Na tuimiliki nchi ambamo Mungu anakaa.”

- 13 Ee Mungu wangu, wafanye wawe kama mchongoma unaopeperushwa,^{*c}

Kama majani makavu yanayopeperushwa na upepo.

- 14 Kama moto unaoteketeza kabisa msitu,

Kama mwali wa moto unaounguzwa milima,^d

- 15 Wafuatie vivyo hivyo kwa tufani yako^e

Na kuwaogopesha kwa dhoruba yako ya upepo.^f

- 16 Funika nyuso zao kwa aibu,^{*}

Ili walitafute jina lako, Ee Yehova.

- 17 Na waaibishwe na kuogopeshwa milele;

Na wafedheheshwe na kuangamia;

- 18 Na watu wajue kwamba wewe, ambaye jina lako ni Yehova,^g

Wewe peke yako ndiye Uliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote.^h

Kwa kiongozi; juu ya Gitithi.*
Muziki wa wana wa Kora.ⁱ

- 84** Jinsi linavyovutia sana* hema lako tukufu la ibada,^j

Ee Yehova wa majeshi!

83:11 *Au “viongozi.” 83:13 *Au “kama mbaruti.” 83:16 *Tnn., “Jaza nyuso zao aibu.” 84:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012. 84:1 *Au “linavyope-ndwa sana.”

SURA YA 83

a Amu 7:25

b Amu 8:21

c Isa 17:13

d Zb 144:5
Nah 1:6

e Isa 30:30

f Zb 11:6

g Kut 6:3
Zb 68:4
Isa 42:8
Isa 54:5

h Zb 59:13
Zb 92:8
Da 4:17

SURA YA 84

i 2Nya 20:19

j Zb 27:4
Zb 43:3
Zb 46:4

Safu ya 2

a Zb 42:1, 2
Zb 63:1, 2

b Zb 23:6
Zb 65:4

c 1Nya 25:7
Zb 150:1

d Zb 28:7

e Zb 18:32
Isa 40:29–31
Hab 3:19

- 2 Nafsi yangu yote inatamani,

Naam, ninazimia kwa kutamani,

Nyua za Yehova.^a

Moyo wangu na mwili wangu humshangilia kwa sauti Mungu aliye hai.

- 3 Hata ndege hupata makao huko

Na mbayuwayu hujipatia kiota,

Ambamo huyatunza maki-nda wake

Karibu na madhabahu yako tukufu, Ee Yehova wa majeshi,

Mfalme wangu na Mungu wangu!

- 4 Wenye furaha ni wale wanaokaa katika nyumba yako!^b

Wanaendelea kukusifu.^c
(Sela)

- 5 Wenye furaha ni watu wanaopata nguvu kutoka kwako,^d

Ambao mioyo yao inatamani sana* barabara kuu.

- 6 Wanapopita katika Bonde la Mibaka,*

Wanalifanya kuwa mahali penye chemchemi;

Na mvua ya mapema huli-lisha[#] baraka.

- 7 Wataendelea kutembea kutoka nguvu hadi nguvu zaidi;^e

Kila mmoja wao hufika mbele za Mungu kule Sayuni.

- 8 Ee Yehova Mungu wa majeshi, isikie sala yangu;

84:5 *Tnn., “inakazia.” 84:6 *Au “bonde lenye vichaka vya mibaka.” [#]Au labda, “Na mfundishaji hujifunika mwenyewe.”

Sikiliza, Ee Mungu wa Yakobo. (*Sela*)

- 9 Tazama, ngao yetu^a na Mungu wetu,*
Utazame uso wa mtiwama-
mafuta wako.^b
- 10 Kwa maana siku moja ka-
tika nyua zako ni bora
kuliko siku elfu moja
kwingineko!^c
Ninachagua kusimama
kwenye kizingiti cha
nyumba ya Mungu
wangu
Badala ya kukaa katika
mahema ya uovu.
- 11 Kwa maana Yehova Mungu
ni jua^d na ngao;^e
Yeye hutoa kibali na
utukufu.
Yehova hatawanyima
jambo lolote jema
Wale wanaotembea kwa
utumilifu.^f
- 12 Ee Yehova wa majeshi,
Mwenye furaha ni mtu
anayekutumaini.^g
Kwa kiongozi.
Muziki wa wana wa Kora.^h
- 85** Ee Yehova, umeionye-
sha kibali nchi yako;ⁱ
Uliwarudisha watu wa
Yakobo waliokuwa wa-
metekwa.^j
- 2 Umelisamehe kosa la watu
wako;
Ulisamehe* dhambi yao
yote.^k (*Sela*)
- 3 Uliizuia ghadhabu yako
yote;
Uliiacha hasira yako kali.^l
- 4 Turudishe,* Ee Mungu wa
wokovu wetu,
Na uache kutukasirikia.^m

84:9 *Au labda, "Itazame ngao yetu, Ee Mungu." 85:2 *Tnn., "Uliifunika." 85:4 *Au "Tukasanye tena."

SURA YA 84

- a Mwa 15:1
b 1Sa 2:10
c Zb 26:8
Zb 27:4
Zb 43:3, 4
d Zb 27:1
Isa 60:19, 20
e Kum 33:29
2Sa 22:3
Zb 144:2
f Zb 34:9
Zb 37:18
g Zb 146:5
Yer 17:7

SURA YA 85

- h 2Nya 20:19
i Law 26:42
Yoe 2:18
j Ezz 2:1
Yer 30:18
Eze 39:25
k Yer 50:20
Mik 7:18
l Zb 103:9
Isa 12:1
m Zb 80:3, 4

Safu ya 2

- a Zb 74:1
Zb 79:5
b Ezz 3:11
Yer 33:10, 11
c Omb 3:22
d Isa 57:19
e Kum 8:17, 18
Zb 78:7
f Isa 46:13
g Zb 72:3
Isa 32:17
h Isa 26:9
Isa 45:8
i Zb 84:11
Yak 1:17
j Law 26:4
Zb 67:6
Isa 25:6
Isa 30:23
k Zb 89:14

SURA YA 86

- l Zb 34:6
Isa 66:2

- 5 Je, utatughadhibikia
milele?^a
Je, utaendelea kukasirika
kizazi baada ya kizazi?
- 6 Je, hutatuhisha tena
Ili watu wako washangilie
kwa sababu yako?^b
- 7 Ee Yehova, tutendee kwa
upendo mshikamanifu,^c
Nawe utupe wokovu wako.
- 8 Nitasikiliza jambo ambalo
Mungu wa kweli Yehova
anasema,
Kwa maana atawaambia
watu wake kuhusu ama-
ni,^d washikamanifu
wake,
Lakini wasianze tena ku-
jiamini kupita kiasi.^e
- 9 Kwa hakika wokovu wake
uko karibu na wale wa-
naomwogopa,^f
Ili utukufu wake ukae kati-
ka nchi yetu.
- 10 Upendo mshikamanifu
utakutana na uaminifu;
Uadilifu utabusiana na
amani.^g
- 11 Uaminifu utachipuka du-
niani,
Na uadilifu utatazama chi-
ni kutoka mbinguni.^h
- 12 Naam, Yehova atatoa kili-
cho chema,^{*i}
Na nchi yetu itazaa mavu-
no yake.^j
- 13 Uadilifu utatembea mbele
zake^k
Na kutengeneza njia kwa
ajili ya hatua zake.
Sala ya Daudi.
- 86** Tega sikio lako,* Ee Ye-
hova, nawe unijibu,
Kwa maana ninateseka
nami ni maskini.^l

85:12 *Au "ufanisi." 86:1 *Au "Inama chini na unisikilize."

- 2** Ulinde uhai wangu, * kwa maana mimi ni mshikamanifu.^a
Mwokoe mtumishi wako anayekutumaini,
Kwa maana wewe ni Mungu wangu.^b
- 3** Nionyeshe kibali, Ee Yehova,^c
Kwa maana ninakulilia wewe mchana kutwa.^d
- 4** Mfanye mtumishi wako ahangilie,
Kwa maana ninakugeukia wewe, * Ee Yehova.
- 5** Kwa maana wewe, Ee Yehova, ni mwema^e na uko tayari kusamehe;^f
Una upendo mwingi mshikamanifu kwa wote wanaokuitia.^g
- 6** Ee Yehova, sikiliza sala yangu;
Na usikilize sihi zangu za kuomba msaada.^h
- 7** Ninakuitia wewe katika siku ninayotaabika,ⁱ
Kwa maana utanijibu.^j
- 8** Hakuna yeyote aliye kama wewe kati ya miungu, Ee Yehova,^k
Hakuna kazi zilizo kama kazi zako.^l
- 9** Mataifa yote uliyoyaumba Yatakuja na kuinama mbele zako, Ee Yehova,^m
Nayo yatalitukuza jina lako.ⁿ
- 10** Kwa maana wewe ni mkuu, nawe unafanya mambo yanayostaajabisha;^o
Wewe ni Mungu, wewe peke yako.^p
- 11** Nifundishe, Ee Yehova, kuhusu njia yako.^q

86:2 *Au "Ilinde nafsi yangu." **86:4** *Au "ninakuinulia wewe nafsi yangu."

SURA YA 86

a Zb 37:28

b 2Nya 16:9

c Zb 57:1

d Zb 25:5

e Zb 25:8
Zb 145:9
Lu 18:19f Isa 55:7
Mik 7:18

g Zb 130:7

h Zb 17:1

i Zb 18:6

j Zb 116:1

k Kut 15:11
Zb 96:5
1Ko 8:5, 6l Kum 3:24
Zb 104:24m Isa 2:2, 3
Zek 14:9
Ufu 7:9, 10

n Ufu 15:4

o Zb 72:18
Da 6:27p Kum 6:4
Zb 83:18
Isa 44:6
1Ko 8:4q Zb 27:11
Zb 119:33
Zb 143:8
Isa 54:13

Safu ya 2

a Zb 43:3

b Mhu 12:13
Yer 32:39

c Mt 22:37

d Ayu 33:28
Zb 56:13
Zb 116:8

e 2Sa 15:12

f Zb 10:4
Zb 54:3g Kut 34:6
Ne 9:17
Yon 4:2

h Zb 25:16

i Zb 28:7

Nitatembea katika kweli yako.^aUnganisha moyo wangu* ili niliogope jina lako.^b

- 12** Ninakusifu, Ee Yehova Mungu wangu, kwa moyo wangu wote,^c

Nami nitalitukuza jina lako milele,

- 13** Kwa maana upendo wako mshikamanifu ni mkuu kwangu,

Nawe umeuokoa uhai wangu* kutoka katika vina vya Kaburi.^{#d}

- 14** Ee Mungu, watu wenye kimbelebele wanainuka dhidi yangu;^e

Kundi la wanaume wakatili wanataka kuniua,*

Nao hawakuheshimu kamwe.^{#f}

- 15** Lakini wewe, Ee Yehova, ni Mungu mwenye rehma na huruma,*

Si mwepesi wa hasira, nawe una upendo mwingi mshikamanifu na uaminifu.^{#g}

- 16** Nigeukie na kunionyesha kibali.^h

Mpe mtumishi wako nguvu zako,ⁱ

Na umwokoe mwana wa kijakazi wako.

- 17** Nionyeshe ishara ya* wema wako,
Ili wale wanaonichukia waione na kuaibika.

Kwa maana wewe, Ee Yehova, ni msaidizi wangu na mfariji wangu.

86:11 *Au "Nipe moyo ambao haujagawanyika." **86:13** *Au "umeiokoa nafsi yangu." #Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. **86:14** *Au "wanaitafuta nafsi yangu." #Au "hawajakuweka mbele yao." **86:15** *Au "neema." #Au "kweli." **86:17** *Au "uthibitisho wa."

Muziki wa wana wa Kora.^a Wimbo.

87 Msingi wa jiji lake uko katika milima mitakatifu.^b

2 Yehova anapenda malango ya Sayuni^c

Kuliko mahema yote ya Yakobo.

3 Mambo matukufu yanasemwa kukuhusu, Ee jiji la Mungu wa kweli.^d (*Sela*)

4 Nitamhesabu Rahabu^e na Babiloni kuwa kati ya wale wanaonijua* mimi; Tazama, Ufilisti na Tiro, pamoja na Kushi.

Itasemwa hivi: "Huyu alizaliwa humo."

5 Na kuhusu Sayuni itasemwa:

"Kila mtu alizaliwa humo." Na Aliye Juu Zaidi atamwimarisha kabisa.

6 Yehova atatangaza hivi atakapoyaandikisha mataifa:

"Huyu alizaliwa humo." (*Sela*)

7 Waimbaji^f na wale wanaocheza dansi za muzunguko^g watasema: "Chemchemi zangu zote zimo ndani yako."^{*h}

Wimbo. Muziki wa wana wa Kora.ⁱ Kwa kiongozi; kwa mtindo wa Mahalathi,^{*} uimbwe kwa zamu. Maskili* ya Hemani/ Mwezra.

88 Ee Yehova, Mungu wa wokovu wangu,^k Wakati wa mchana ninalia kwa sauti,

Na usiku ninakuja mbele zako.^l

2 Sala yangu na ikufikie,^m

87:4 *Au "wanaonitambua." 87:7 *Au "Kwangu mimi, wewe ni chanzo cha vitu vyote." 88:Uta; 88:3 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 87

a 2Nya 20:19

b Zb 48:1

c Zb 78:68
Zb 132:13

d Zb 48:2
Isa 60:14

e Zb 89:10
Isa 30:7

f 1Nya 15:16

g Zb 150:4

h Zb 46:4

SURA YA 88

i 2Nya 20:19

j 1Fa 4:30, 31
1Nya 2:6

k Zb 27:9
Isa 12:2

l Zb 22:2

m 1Fa 8:30

Safu ya 2

a Zb 141:1

b Zb 71:20

c Isa 38:10

d Zb 143:7

e Zb 31:12

f Zb 90:7
Zb 102:10

g Ayu 19:13, 19
Zb 31:11
Zb 142:4

h Ayu 17:7
Zb 42:3
Omb 3:49

i Zb 55:17

Tega sikio lako* usikie kilio changu cha kuomba msaada.^a

3 Kwa maana nafsi* yangu imejaa msiba,^b

Na uhai wangu uko kwenye kingo za Kaburi.^{#c}

4 Tayari nimehesabiwa miongoni mwa wale wanaoshuka shimoni;^{*d} Nimekuwa mtu asiye na uwezo wowote,^{#e}

5 Aliyeachwa kati ya watu waliokufa

Kama walioauwa wanaola-

la kaburini, Ambao huwakumbuki

tena Na ambao wametengwa mbali na utunzaji* wako.

6 Umeniweka katika shimo lenye kina kirefu sana, Sehemu zenye giza, shimo kubwa.*

7 Ghadhabu yako inanilemea sana,^f

Nawe unanilemea kwa mawimbi yako yenye nguvu. (*Sela*)

8 Umewafukuza rafiki zangu mbali sana nami;^g

Umenifanya niwe kitu kinachowachukiza.

Nimenaswa na siwezi kutoroka.

9 Jicho langu limedhoofika kwa sababu ya mateso yangu.^h

Ee Yehova, ninakulilia

mchana kutwa;ⁱ Ninakunyooshea mikono yangu.

88:2 *Au "Inama chini na unisikilize." 88:3 #Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 88:4 *Au "kaburini." #Au "mtu asiye na nguvu." 88:5 *Tnn., "mkono." 88:6 *Au "abiso." Angalia Kamusi, uku. 2012.

- 10** Je, utawatendea maajabu waliokufa?
Je, wale waliokufa ambao hawana uwezo wanaweza kuinuka na kukusifu?^a (*Sela*)
- 11** Je, upendo wako mshikamanifu utatangazwa kaburini,
Na uaminifu wako mahali pa maangamizi?^{*}
- 12** Je, maajabu yako yatajulikana gizani
Au uadilifu wako katika nchi ya waliosahauliwa?^b
- 13** Lakini bado ninakulilia unisaidie, Ee Yehova,^c
Kila asubuhi sala yangu inakufikia.^d
- 14** Kwa nini, Ee Yehova, unanikataa?^{*e}
Kwa nini unanificha uso wako?^f
- 15** Tangu nilipokuwa kijana, Nimeteseka nami niko karibu kuangamia;^g
Nimekufa ganzi kwa sababu ya mambo yanayotisha unayoruhusu yanipate.
- 16** Hasira yako inayowaka inanilemea;^h
Vitisho vyako vinaniangamiza.
- 17** Vinanizunguka mchana kutwa kama maji;
Vinanizingira ili kunibana pande zote.^{*}
- 18** Umewafukuza rafiki zangu na wenzangu mbali sana nami;ⁱ
Giza limekuwa mwenzangu.

88:11 *Au "katika Abadoni." **88:14**
*Au "unaikataa nafsi yangu." **88:17**
*Au labda, "Vinanizingira vyote kwa pamoja."

SURA YA 88

a Ayu 14:14
Zb 115:17
Isa 38:18

b Mhu 2:16
Mhu 8:10
Mhu 9:5

c Zb 46:1

d Zb 55:17
Zb 119:147

e Zb 43:2

f Ayu 13:24
Zb 13:1

g Ayu 17:1

h Zb 102:10

i Ayu 19:13
Zb 31:11
Zb 38:11
Zb 142:4

Safu ya 2

SURA YA 89

a 1Fa 4:30, 31
1Nya 2:6

b 1Nya 16:41
Isa 54:10

c 2Sa 7:8
1Fa 8:16
Lu 1:32, 33

d Zb 132:11
Eze 34:23
Ho 3:5
Yoh 7:42

e 1Nya 17:11
Ufu 22:16

f 2Sa 7:12, 13
Ebr 1:8

g Zb 40:5
Zb 71:19

h Ayu 38:7

i Isa 6:2, 3

j Da 7:9, 10

k 1Sa 2:2
Zb 84:12

l Kum 32:4

Maskili.* Wa Ethani^a Mwezra.

- 89** Nitaimba kuhusu jinsi Yehova anavyoonyesha upendo mshikamanifu milele.
Kwa kinywa changu ninatangazia vizazi vyote uaminifu wako.
- 2** Kwa maana nimesema:
"Upendo mshikamanifu utajengwa* milele,^b
Nawe umeuimarisha kabisa uaminifu wako mbinguni."
- 3** "Nimefanya agano pamoja na yule niliyemchagua;^c
Nimemwapa Daudi mtumishi wangu;^d
- 4** 'Nitauimarisha kabisa uzao wako*^e milele,
Nami nitakijenga kiti chako cha ufalme kwa vizazi vyote.'"^f (*Sela*)
- 5** Mbingu zinasifu maajabu yako, Ee Yehova,
Naam, uaminifu wako katika kutaniko la watakatifu.
- 6** Kwa maana ni nani mbinguni anayeweza kulinganishwa na Yehova?^g
Ni nani miongoni mwa wana wa Mungu^h aliye kama Yehova?
- 7** Mungu anaogopwa katika baraza* la watakatifu;ⁱ
Yeye ni mtukufu na mwenye kuogopesha kwa wote wanaomzunguka.^j
- 8** Ee Yehova Mungu wa majeshi,
Ni nani aliye na nguvu kama wewe, Ee Yah?^k
Uaminifu wako unakuzunguka.^l

89:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.
89:2 *Au "utadumu." **89:4** *Tnn., "Nitaiimarisha kabisa mbegu yako." **89:7**
*Au "kusanyiko."

- 9 Unautawala msukosuko wa bahari;^a
Mawimbi yake yanapoinu-ka, unayatuliza.^b
- 10 Umemponda Rahabu^c kama mtu aliyeuawa.^d
Kwa mkono wako wenye nguvu umewatawanya maadui wako.^e
- 11 Mbingu ni zako, na dunia ni yako;^f
Nchi inayozaa na vinavyoi-
jaza^g—umeviumba.
- 12 Kaskazini na kusini—uli-
ziumba;
Tabori^h na Hermoniⁱ hu-
lisifu kwa shangwe jina
lako.
- 13 Mkono wako una uwezo;^j
Mkono wako una nguvu;^k
Mkono wako wa kuume
umekwezwa.^l
- 14 Uadilifu na haki ndio msi-
ngi wa kiti chako cha
ufalme;^m
Upendo mshikamanifu
na uaminifu husimama
mbele zako.ⁿ
- 15 Wenye furaha ni watu
wanaojua kelele za sha-
ngwe.^o
Ee Yehova, wanatembea
katika nuru ya uso wako.
- 16 Wanashangilia mchana
kutwa kwa sababu ya
jina lako,
Na kwa sababu ya uadilifu
wako wanakwezwa.
- 17 Kwa maana wewe ni utu-
kufu wa nguvu zao,^p
Na kwa kibali chako nguvu
zetu zinakwezwa.^{*q}
- 18 Kwa maana ngao yetu ni
ya Yehova,
Mfalme wetu ni wa Mtaka-
tifu wa Israeli.^r
- 19 Wakati huo uliwaambia

89:17 *Tnn., "pembe yetu inakwezwa."

SURA YA 89

a Yer 31:35

b Zb 65:7
Zb 107:29

c Isa 30:7

d Kut 14:26
Kut 15:4

e Kut 3:20
Kum 4:34
Lu 1:51

f 1Ko 10:26

g 1Nya 29:11
Zb 50:12

h Yos 19:22, 23

i Kum 3:8
Yos 12:1

j Kut 6:6

k Kut 13:3

l Zb 44:3

m Kum 32:4
Zb 71:19
Ufu 15:3

n Kut 34:6
Yer 9:24

o Hes 10:10
Zb 98:6

p Zb 28:7

q 1Sa 2:10

r Zb 2:6

Safu ya 2

a 1Sa 18:14

b 2Sa 7:8

c Mdo 13:22

d 1Sa 16:12, 13
Mdo 10:38

e Zb 80:17
Isa 42:1

f 1Nya 17:9

g 2Sa 3:1
2Sa 7:9

h Zb 110:1

i 2Sa 7:15
1Nya 17:13
Mdo 13:34

j 1Fa 4:21
Zb 72:8

k 2Sa 22:47
Zb 18:2

l Zb 2:7
Ebr 1:5

m 1Ti 6:15
Ufu 1:5
Ufu 19:16

n Mdo 13:34

- hivi washikamanifu wako katika maono:
"Nimempa nguvu aliye hodari;^a
Nimemkweza aliyechaguli-
wa kutoka miongoni
mwa watu.^b
- 20 Nimempata Daudi mtumi-
shi wangu;^c
Kwa mafuta yangu
matakatifu nimemtia
mafuta.^d
- 21 Mkono wangu utamtege-
meza,^e
Na mkono wangu utamwi-
marisha.
- 22 Hakuna adui atakayemto-
za ushuru,
Na hakuna mwovu ataka-
yemkandamiza.^f
- 23 Nitawavunja maadui wake
vipandevipande kutoka
mbele yake^g
Na kuwaangamiza wale
wanaomchukia.^h
- 24 Uaminifu wangu na
upendo wangu mshika-
manifu uko pamoja
naye,ⁱ
Na katika jina langu nguvu
zake zitakwezwa.^{*}
- 25 Nitauweka mkono wake*
juu ya bahari
Na mkono wake wa kulia
juu ya mito.^j
- 26 Atasema kwa sauti: 'Wewe
ni Baba yangu,
Mungu wangu na Mwamba
wa wokovu wangu.'^k
- 27 Nami nitamfanya kuwa
mzaliwa wa kwanza,^l
Aliye juu zaidi kati ya
wafalme wa dunia.^m
- 28 Nitadumisha upendo
wangu mshikamanifu
kumwelekea milele,ⁿ

89:24 *Tnn., "pembe yake itakwezwa."

89:25 *Au "Nitaweka mamlaka yake."

Na agano langu nililofanya pamoja naye halitavunjika kamwe.^a

29 Nitauimarisha uzao wake* milele

Na kukifanya kiti chake cha ufalme kidumu kama mbingu.^b

30 Wanawe wakiacha sheria yangu

Na wasipotembea kulingana na maagizo yangu,*

31 Wakizivunja sheria zangu Na wasiposhika amri zangu,

32 Basi nitaadhibu uasi wao* kwa fimbo^c

Na kosa lao kwa viboko.

33 Lakini sitaacha kamwe kumtendea kwa upendo wangu mshikamanifu^d

Wala sitakosa kutimiza ahadi yangu.*

34 Sitavunja agano langu^e Wala kubadili maneno ya-liyosemwa na midomo yangu.^f

35 Nimeapa katika utakatifu wangu, mara moja kwa wakati wote; Sitamwambia Daudi uwongo.^g

36 Uzao wake utadumu* milele;^h

Kiti chake cha ufalme kitadumu kama jua mbele zangu.ⁱ

37 Kama mwezi, kitaimarishwa kabisa milele Kama shahidi mwaminifu angani." (*Sela*)

38 Lakini wewe mwenyewe

89:29 *Tnn., "Nitaiimarisha mbegu yake." **89:30** *Au "hukumu zangu." **89:32** *Au "kutotii kwao." **89:33** *Tnn., "Wala kuwa mwongo kuhusu uaminifu wangu." **89:36** *Tnn., "Mbegu yake itadumu."

SURA YA 89

a 2Sa 23:5
Zb 89:34

b Isa 9:7
Yer 33:17
Ebr 1:8

c 2Sa 7:14
1Fa 11:14, 31

d 2Sa 7:15
1Fa 11:32, 36

e Yer 33:20, 21

f Yak 1:17

g Hes 23:19
Zb 132:11

h 2Sa 7:16, 17
Zb 72:17
Isa 11:1
Yer 23:5
Yoh 12:34
Ufu 22:16

i Da 7:14
Lu 1:32, 33

Safu ya 2

a 1Nya 28:9

b Kum 28:37

c Kum 28:25

d Zb 13:1

e Ayu 7:7
Zb 39:5

f Ayu 30:23
Zb 49:7, 9

umemtupa mbali na kumkataa;^a

Umekasirikia sana mtiwa-mafuta wako.

39 Umelikataa kwa dharau agano ulilofanya na mtu-mishi wako;

Umelichafua* taji lake kwa kulitupa ardhini.

40 Umezivunja kuta zake zote za mawe;*

Umezifanya ngome zake kuwa magofu.

41 Wote wanaopita karibu naye wamempora;

Yeye ni shutuma kwa jirani zake.^b

42 Umewapa ushindi wapi-nzani wake;*^c

Umewafanya maadui wake wote washangilie.

43 Pia umeusukuma nyuma upanga wake,

Na kumfanya ashindwe vitani.

44 Umekomesha fahari yake Na kukitupa ardhini kiti chake cha ufalme.

45 Umefupisha siku zake za ujana;

Umemvisha aibu. (*Sela*)

46 Ee Yehova, utaendelea kujificha mpaka lini? Utajificha milele?^d

Je, ghadhabu yako itaendelea kuwaka kama moto?

47 Kumbuka jinsi maisha yangu yalivyo mafupi!^e

Je, uliwaumba wanadamu wote bila kusudi?

48 Ni mwanadamu gani anayeweza kuishi na asione kifo kamwe?^f

89:39 *Au "Umelitia unajisi." **89:40** *Au "Umeyavunja mabanda yake yote ya mawe." **89:42** *Tnn., "Umekuina juu mkono wa kulia wa maadui wake."

Je, anaweza kujiokoa mwenyewe* kutoka katika nguvu za Kaburi?# (Sela)

49 **Yako wapi matendo yako ya zamani ya upendo mshikamanifu, Ee Yehova,**

Ambayo ulimwambia Daudi katika uaminifu wako?^a

50 **Kumbuka, Ee Yehova, dhi-**

89:48 *Au "kuiokoa nafsi yake." #Tnn., "mkono wa Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 89

a 2Sa 7:12-15
Zb 132:11
Isa 55:3

Safu ya 2

a Zb 41:13
Zb 72:18

haka ambazo watumishi wako wanavurumishiwa; Jinsi ninavyolazimika kuvumilia* dhahaka za mataifa yote;

51 **Jinsi ambavyo maadui wako wamevurumisha matusi, Ee Yehova; Jinsi ambavyo wameitukana kila hatua ya mtiwa-mafuta wako.**

52 **Yehova na asifiwe milele. Amina na Amina.^a**

89:50 *Tnn., "kubeba kifuani mwangu."

KITABU CHA NNE
(Zaburi 90-106)

Sala ya Musa, mtu wa Mungu wa kweli.^a

90 **Ee Yehova, umekuwa makao yetu*^b katika vizazi vyote.**

2 **Kabla milima haijazaliwa Au kabla hujaiumba* dunia na nchi inayozaa,^c Tangu milele hadi milele, wewe ni Mungu.^d**

3 **Unamfanya mwanadamu anayeweza kufa arudi mavumbini; Unasema: "Rudini, enyi wanadamu."^e**

4 **Kwa maana miaka elfu moja machoni pako ni kama siku ya jana ambayo tayari imepita,^f Kama kesha moja tu la usiku.**

5 **Unawafagilia mbali;^g wanakuwa kama usingizi tu; Asubuhi, wao ni kama majani yanayochipuka.^h**

6 **Asubuhi yanachanua maua na kusitawi,**

SURA YA 90

a Kum 33:1

b Kum 33:27
Zb 91:1

c Yer 10:12

d Zb 93:2
Isa 40:28
Hab 1:12
ITI 1:17
Ufu 1:8
Ufu 15:3

e Mwa 3:19
Zb 104:29
Zb 146:3, 4
Mhu 3:20
Mhu 12:7

f 2Pe 3:8

g Ayu 9:25

h Zb 103:15
1Pe 1:24

Safu ya 2

a Ayu 14:2

b Hes 17:12, 13
Kum 32:22

c Yer 16:17

d Met 24:12
Ebr 4:13

e 2Sa 19:34, 35

f Ayu 14:10
Zb 78:39
Lu 12:20
Yak 4:13, 14

Lakini ifikapo jioni yame-nyauka na kukauka.^a

7 **Kwa maana tumemezwa na hasira yako^b**

Na kutishwa na ghadhabu yako.

8 **Unayaweka makosa yetu mbele zako;^{*c}**

Siri zetu zinafichuliwa na nuru ya uso wako.^d

9 **Siku zetu zinadidimia* kwa sababu ya ghadhabu yako;**

Na miaka yetu hufikia kikomo kama mnong'ono.[#]

10 **Urefu wa maisha yetu ni miaka 70,**

Au miaka 80^e ikiwa mtu ana nguvu za pekee.*

Lakini imejaa taabu na huzuni;

Nayo hupita haraka, nasi hutokomea.^f

11 **Ni nani anayeweza kuelewa nguvu za hasira yako?**

90:8 *Au "Unajua makosa yetu." 90:9 *Au "Maisha yetu yanadidimia." #Au "kupiga kite." 90:10 *Au "kwa sababu ya uwezo wa pekee."

90:1 *Au labda, "kimbilio letu." 90:2 *Au "hujatokeza kama kwa uchungu wa kuzaa."

Ghadhabu yako ni kubwa kama hofu unayostahili kuonyeshwa.^a

12 Tufundishe jinsi ya kuhesabu siku zetu^b

Ili tupate moyo wa hekima.

13 Rudi, Ee Yehova!^c Hali hiyo itadumu mpaka lini?^d

Wahurumie watumishi wako.^e

14 Tushibishe asubuhi kwa upendo wako mshikamifu,^f

Ili tupaze sauti kwa shangwe na kushangilia^g siku zetu zote.

15 Tufanye tushangilie kulingana na siku ambazo umetutesa,^h

Kwa kadiri ya miaka mingi tuliyopata msiba.ⁱ

16 Watumishi wako na waone utendaji wako, Na wana wao waone fahari yako.^j

17 Kibali chako, Ee Yehova Mungu wetu, na kiwe juu yetu;

Na uifanikishe* kazi ya mkono yetu.

Naam, ifanikishe# kazi ya mikono yetu.^k

91 Yeyote anayekaa mahali pa siri pa Aliye Juu Zaidi^l

Ataishi katika kivuli cha Mweza-Yote.^m

2 Nitamwambia Yehova: "Wewe ni kimbilio langu na ngome yangu,ⁿ Mungu wangu ninayemtumaini."^o

3 Kwa maana atakuokoa usinaswe na mtego wa mwindaji wa ndege,

SURA YA 90

a Isa 33:14

Lu 12:5

b Zb 39:4

c Zb 6:4

d Zb 89:46

e Kum 32:36

Zb 135:14

f Zb 36:7

Zb 51:1

Zb 63:3

Zb 85:7

g Zb 149:2

h Zb 30:5

i Kum 2:14

j Hes 14:31

Yos 23:14

k Zb 127:1

Met 16:3

Isa 26:12

1Ko 3:7

SURA YA 91

l Zb 27:5

Zb 31:20

Zb 32:7

m Zb 57:1

n Zb 18:2

Met 18:10

o Met 3:5

Safu ya 2

a Kut 19:4

Kum 32:11

Ru 2:12

b Zb 57:3

Zb 86:15

c Mwa 15:1

Zb 84:11

d Zb 121:4, 6

Isa 60:2

e Zb 64:2, 3

Isa 54:17

f Kut 12:13

g Zb 71:3

Zb 90:1

h Met 12:21

i 2Fa 6:17

Zb 34:7

Mt 18:10

j Kut 23:20

Ebr 1:7, 14

k Isa 63:9

Kutoka kwa ugonjwa wa kuambukiza unaoangamiza.

4 Kwa manyoya yake ataku- funika,

Nawe utapata kimbilio chini ya mabawa yake.^a

Uaminifu wake^b utakuwa ngao kubwa^c na ukuta wa ulinzi.*

5 Hutaogopa vitisho vya usiku,^d

Wala mshale unaoruka mchana,^e

6 Wala ugonjwa wa kuambukiza unaonyemelea gizana,

Wala maangamizi yanayoharibu wakati wa adhuhuri.

7 Eلفu moja wataanguka kando yako

Na elfu kumi mkono wako wa kulia,

Lakini hayatakukaribia wewe.^f

8 Utayaona tu kwa macho yako

Unaposhuhudia adhabu* ya waovu.

9 Kwa sababu ulisema: "Yehova ni kimbilio langu," Umemfanya Aliye Juu Zaidi kuwa makao* yako;^g

10 Hutapatwa na msiba,^h Na hakuna pigo litakalokaribia hema lako.

11 Kwa maana atawaagiza malaika zakeⁱ kukuhusu wewe, Ili kukulinda katika njia zako zote.^j

12 Watakubeba mikononi mwao,^k

91:4 *Au "boma." **91:8** *Tnn., "malipo." **91:9** *Au labda, "ngome; kimbilio."

90:17 *Au "uimarisha kabisa." #Au "jimarisha kabisa."

Ili mguu wako usigonge
jiwe.^a

- 13** Utamkanyaga mwanasi-
mba na swila;
Utamkanyagia chini simba
mwenye manyoya mare-
fu shingoni na nyoka
mkubwa.^b
- 14** Mungu alisema: “Kwa
sababu ananipenda,^{*}
nitamwoko.^c
Nitamlinda kwa sababu
analijua[#] jina langu.^d
- 15** Ataniita, nami nitamjibu.^e
Nitakuwa pamoja naye ka-
tika taabu.^f
Nitamwoko na kumtu-
kuza.
- 16** Nitamshibisha kwa mai-
sha marefu,^g
Nami nitamfanya aone
matendo yangu ya
wokovu.”^h

Muziki. Wimbo wa siku ya Sabato.

- 92** Ni vema kukushukuru,
Ee Yehovaⁱ
Na kuliimbua sifa^{*} jina
lako, Ee Uliye Juu Zaidi,
2 Kutangaza upendo wako
mshikamanifu/ asubuhi
Na uaminifu wako nyakati
za usiku,
3 Kwa kinanda cha nyuzi
kumi na kwa udi,
Kwa sauti tamu ya kinubi.^k
4 Kwa maana umenifanya
nishangilie, Ee Yehova,
kwa sababu ya matendo
yako;
Kwa sababu ya kazi za
mikono yako ninapaza
sauti kwa shangwe.
5 Jinsi kazi zako zilivyo
kuu, Ee Yehova!^l

91:14 *Tnn., “amejiunga nami.” #Au
“analitambua.” 91:16 *Au “aone woko-
vu kutoka kwangu.” 92:1 *Au “kulipi-
gia muziki.”

SURA YA 91

a Zb 37:24
Mt 4:6
Lu 4:10, 11

b Lu 10:19

c Zb 18:2

d Zb 9:10
Met 18:10

e Ro 10:13
Ebr 5:7

f Zb 138:7
Isa 43:2

g Zb 21:1, 4
Met 3:1, 2

h Isa 45:17

SURA YA 92

i Zb 50:23

j Isa 63:7

k 1Nya 15:16
1Nya 25:6
2Nya 29:25

l Zb 40:5
Zb 145:4
Mhu 3:11
Ufu 15:3

Safu ya 2

a Ayu 26:14
Ro 11:33

b Zb 14:1
1Ko 2:14

c Zb 37:35, 38
Yer 12:1-3

d Kum 28:7
Zb 68:1

e Zb 23:5

f Zb 37:34

g Zb 52:8
Isa 61:3
Isa 65:22

h Zb 100:4

i Zb 71:18
Met 16:31
Isa 40:31
Isa 46:4

Jinsi mawazo yako yalivyo
na kina sana!^a

- 6** Mtu yeyote asiyetumia
akili hawezi kuyajua;
Na hakuna mtu yeyote mji-
nga anayeweza kuelewa
hili.^b
- 7** Waovu wanapochipuka
kama magugu^{*}
Na watenda mabaya wote
wanapositawi,
Ni ili waangamizwe
milele.^c
- 8** Lakini wewe umekwezwa
milele, Ee Yehova.
- 9** Kwa kweli, watazame ma-
dui wako wakishindwa,
Ee Yehova,
Tazama jinsi maadui wako
watakavyoangamia;
Watenda maovu wote wa-
tatawanywa.^d
- 10** Lakini utazikweza nguvu
zangu kama za^{*} fahali
mwitu;
Nitailainisha ngozi yangu
kwa mafuta mapya.^e
- 11** Macho yangu yatawaa-
ngalia maadui wangu
wakishindwa;^f
Masikio yangu yatasikia
kuhusu kuangamia kwa
watu waovu wanaonisha-
mbulia.
- 12** Lakini waadilifu watasita-
wi kama mtende
Na kuwa wakubwa kama
mwerezi kule Lebanoni.^g
- 13** Wamepandwa katika nyu-
mba ya Yehova;
Wanasitawi katika nyua za
Mungu wetu.^h
- 14** Hata wakati wa uzeeni^{*}
wataendelea kunawiri;ⁱ

92:7 *Au “majani.” 92:10 *Tnn., “utai-
kweza pembe yangu kama ya.” 92:14
*Au “wakiwa na mvi.”

Wataendelea kuwa na nguvu* na kuwa wabichi,^a

15 Wakitangaza kwamba Yehova ni mnyoofu.

Yeye ni Mwamba wangu,^b ambaye hana ukosefu wowote wa uadilifu.

93 Yehova amekuwa Mfalme!^c

Amevaa adhama; Yehova amevaa nguvu; Huzivaa kama mshipi. Dunia imeimarishwa kabisa;

Haiwezi kusogezwa.*

2 Kiti chako cha ufalme kilimarishwa kabisa zamani za kale;^d

Umekuwapo tangu milele.^e

3 Mito imefurika, Ee Yehova,

Mito imefurika na kunguruma;

Mito inaendelea kufurika na kugonga kwa kishindo.

4 Ana nguvu kuliko sauti ya maji mengi,

Ana nguvu kuliko mawimbi makubwa ya bahari,^f Yehova ni mwenye fahari mbinguni.^g

5 Vikumbusho vyako vinategemeka sana.^h

Utakatifu unaipamba* nyumba yako nyakati zote,ⁱ Ee Yehova.

94 Ee Mungu wa kisasi, Yehova,^j

Ee Mungu wa kisasi, angaza!

2 Inuka, Ee Mwamuzi wa dunia.^k

Walipe wanachostahili watu wenye kiburi.^l

92:14 *Tnn., "kuwa wanene." 93:1 *Au "kutikiswa." 93:5 *Au "unaifaa."

SURA YA 92

a Yer 17:7, 8

b Kum 32:4

SURA YA 93

c Zb 96:10

Zb 97:1

Isa 52:7

Ufu 11:17

Ufu 19:6

d Zb 145:13

e Zb 90:2

f Zb 65:7

g Zb 8:1

Zb 76:4

h Zb 19:7

Zb 119:111

i Eze 43:12

1Pe 1:16

SURA YA 94

j Kum 32:35

Nah 1:2

Ro 12:19

k Mwa 18:25

Mdo 17:31

l Zb 31:23

Safu ya 2

a Zb 73:3

Zb 74:10

b Zb 14:4

c Zb 59:2, 7

Eze 8:12

d Zb 10:4, 11

Zb 73:3, 11

Isa 29:15

e Met 1:22

f Zb 34:15

g Zb 9:5

Isa 10:12

h Zb 25:8

Isa 28:26

Yoh 6:45

i 1Ko 3:20

j Zb 119:71

Met 3:11

1Ko 11:32

Ebr 12:5, 6

k Zb 19:8

l Zb 55:23

2Pe 2:9

m 1Sa 12:22

Zb 37:28

Ebr 13:5

3 Waovu wataendelea mpa-ka lini, Ee Yehova, Waovu wataendelea mpa-ka lini kushangilia?^a

4 Wanaropoka na kuongea kwa kiburi;

Watenda dhambi wote wanajigamba kujihusu.

5 Wanawapanda watu wako, Ee Yehova,^b Na kuukandamiza urithi wako.

6 Wanamuua mjane na mkaaji mgeni, Na kuwaua mayatima.

7 Wanasema: "Yah haoni;^c Mungu wa Yakobo hata- mbui jambo hilo."^d

8 Eleweni jambo hili, ninyi msiotumia akili; Ninyi wajinga, ni lini mta- kapoonyesha ufahamu?^e

9 Yule aliyetengeneza* siki- o, je, hawezi kusikia? Yule aliyeumba jicho, je, hawezi kuona?^f

10 Yule anayeyarekebisha mataifa, je, hawezi kuka- ripia?^g

Yeye Ndiye anayewafundi- sha watu ujuzi!^h

11 Yehova anajua mawazo ya wanadamu, Ya kwamba ni pumzi tu.ⁱ

12 Mwenye furaha ni mtu unayemrekebisha, Ee Yah,^j

Unayemfundisha kwa she- ria yako,^k

13 Ili kumpa utulivu katika siku za msiba, Mpaka shimo litakapochi- mbwa kwa ajili ya mwovu.^l

14 Kwa maana Yehova hata- waacha watu wake,^m

94:9 *Tnn., "aliyelipanda."

Wala hatautupa urithi wake.^a

- 15 Kwa maana kwa mara nyingine tena hukumu itakuwa ya uadilifu, Na wote walio wanyoofu moyoni wataifuata.
- 16 Ni nani atakayeinuka dhidi ya waovu kwa ajili yangu? Ni nani atakayenitetea dhidi ya watenda maovu?
- 17 Ikiwa Yehova hangekuwa msaidizi wangu, Ninge kuwa nimeangamia upesi.^{*b}
- 18 Niliposema: “Mguu wangu unateleza,” Upendo wako mshikamififu, Ee Yehova, uliendelea kunitege-meza.^c
- 19 Mahangaiko* yaliponilemea,[#] Ulinifariji na kunibembeleza.^{△d}
- 20 Je, kiti cha ufalme* chenye ufisadi kinaweza kuungana nawe Wakati kinapotunga matatizo kwa kutumia sheria?^{#e}
- 21 Wanamshambulia vikali mwadilifu? Na kumhukumu asiye na hatia auawe.^{*g}
- 22 Lakini Yehova atakuwa kimbilio langu salama,* Mungu wangu ni mwamba wangu ninaokimbilia.^h

94:17 *Tnn., “nimekaa katika ukimya.”

94:19 *Au “Mawazo yenye kufadhaisha.” #Au “yalipokuwa mengi ndani yangu.” ^Au “Faraja zako ziliibembeleza nafsi yangu.” 94:20 *Au “watawala; mahakimu.” #Au “kwa kutoa amri.”

94:21 *Tnn., “Na damu ya asiye na hatia wanaitangaza kuwa na hatia (ovu).” 94:22 *Au “kilele changu salama.”

SURA YA 94

a Kum 32:9

b Zb 124:2, 3
2Ko 1:10

c 1Sa 2:9
Zb 37:24
Zb 121:3
Omb 3:22

d Zb 86:17
Flp 4:6, 7

e Isa 10:1
Da 6:7
Mdo 5:27, 28

f Zb 59:3

g 1Fa 21:13

h Zb 18:2

Safu ya 2

a Met 5:22
2Th 1:6

b 1Sa 26:9, 10

SURA YA 95

c 2Sa 22:47

d Zb 50:23
Zb 100:4

e Kut 18:11
Yer 10:10
1Ko 8:5, 6

f Amo 4:13
Amo 9:3

g Yer 5:22

h Mwa 1:9, 10

i Zb 100:3
Mt 4:10
Ufu 14:7

j Zb 23:1
Isa 40:11

k Ebr 3:7-11
Ebr 4:7

l Ebr 3:15

- 23 Atafanya matendo yao maovu yawarudie.^a Atawaangamiza* kwa uovu wao wenyewe. Yehova Mungu wetu atawaangamiza.^{#b}

95 Njoooni, na tumshangilie Yehova kwa sauti! Na tumpazie sauti kwa ushindi Mwamba wetu wa wokovu.^c

2 Twendeni mbele zake* tukiwa na shukrani;^d Na tuimbe na kumpazia sauti kwa ushindi.

3 Kwa maana Yehova ni Mungu mkuu, Mfalme mkuu juu ya miungu mingine yote.^e

4 Sehemu zenye kina za dunia zimo mkononi mwake;

Vilele vya milima ni vyake.^f

5 Bahari, ambayo aliiumba, ni yake,^g Na mikonono yake ilitengeneza nchi kavu.^h

6 Njoooni, tuabudu na kuitama;

Na tupige magoti mbele za Yehova Muumba wetu.ⁱ

7 Kwa maana yeye ni Mungu wetu, Na sisi ni watu wa malisho gake,

Kondo anaowatunza.^{*j}

Leo ikiwa mtaisikiliza sauti yake,^k

8 Msiufanye moyo wenu kuwa mgumu kama mliyoyofanya kule Meriba,^{*l}

94:23 *Tnn., “Atawanyamazisha.” #Tnn., “atawanyamazisha.” 95:2 *Tnn., “mbele za uso wake.” 95:7 *Tnn., “wa mkono wake.” 95:8 *Maana yake “Kugombana.”

Kama katika siku ya Masa*
kule nyikani,^a

9 Mababu zenu waliponija-
ribu;^b

Waliniipima, ingawa wali-
kuwa wameona matendo
yangu.^c

10 Kwa miaka 40 nilichu-
kizwa na kizazi hicho,
nikasema:

“Wao ni watu wanaopoto-
ka sikuzote katika mioyo
yao;

Hawajazijua njia zangu.”

11 Kwa hiyo niliapa kwa hasi-
ra yangu:

“Hawataingia katika
pumziko langu.”^d

96 Mwimbieni Yehova
wimbo mpya.^e

Mwimbieni Yehova, dunia
yote!^f

2 Mwimbieni Yehova; lisifu-
ni jina lake.

Tangazeni habari njema za
wokovu wake siku baada
ya siku.^g

3 Tangazeni utukufu wake
miongoni mwa mataifa,
Kazi zake zinazostaajabi-
sha miongoni mwa
mataifa yote.^h

4 Yehova ni mkuu na ana-
stahili kusifiwa kuliko
wote.

Anaogopesha kuliko miu-
ngu mingine yote.

5 Miungu yote ya mataifa ni
miungu ya ubatili,ⁱ

Lakini Yehova ndiye aliye-
ziumba mbingu.^j

6 Mbele zake kuna utukufu*
na fahari;^k

Nguvu na uzuri umo maha-
li pake patakatifu.^l

95:8 *Maana yake “Kujaribu; Jaribu.”

96:6 *Au “adhama.”

SURA YA 95

a Kut 17:7

b Zb 78:18
1Ko 10:9

c Hes 14:22, 23

d Mwa 2:3
Hes 14:22, 23
Ebr 4:3

SURA YA 96

e Zb 33:3

Zb 40:3
Zb 98:1
Zb 149:1

Isa 42:10

f 1Nya 16:23-25

Zb 66:4

g Zb 40:10

Zb 71:15
Isa 52:7

h Mt 28:19

1Pe 2:9
Ufu 14:6

i Zb 97:7

Isa 44:10

j 1Nya 16:26

1Ko 8:4

k Kut 24:9, 10

Isa 6:1-3
Eze 1:27, 28
Ufu 4:2, 3

l 1Nya 16:27

1Nya 29:11

Safu ya 2

a 1Nya 16:28-33

Zb 29:1

b Zb 29:2

Zb 72:19

c Zb 93:1

Zb 97:1
Ufu 11:15
Ufu 19:6

d Zb 67:4

Zb 98:9

e Zb 98:7

f Zb 65:13

g 1Nya 16:33

h Mwa 18:25

Zb 9:8

Zb 98:9

Mdo 17:31

2Pe 3:7

i Kum 32:4

7 Mpeni Yehova anachosta-
hili, enyi familia za
mataifa,

Mpeni Yehova anachosta-
hili kwa sababu ya
utukufu wake na
nguvu zake.^a

8 Mpeni Yehova utukufu
ambao jina lake linasta-
hili;^b

Leteni zawadi na mwingie
katika nyua zake.

9 Mwinamieni* Yehova
katika mapambo mata-
katifu;^c

Tetemekeni mbele zake,
dunia yote!

10 Tangazeni miongoni mwa
mataifa: “Yehova ameku-
wa Mfalme!^c

Dunia imeimarishwa kabi-
sa, haiwezi kusogezwa.*

Atayahukumu[#] mataifa
kwa haki.”^d

11 Mbingu na zishangilie, du-
nia na iwe na shangwe;
Bahari na ingurume na
vitu vyote vinavyoijaza;^e

12 Mashamba na vitu
vyote vilivyomo na
vishangilie.^f

Wakati uleule miti yote
ya msituni na ishangilie
kwa sauti^g

13 Mbele za Yehova, kwa
maana anakuja,*
Anakuja kuihukumu
dunia.

Ataihukumu kwa uadilifu
dunia inayokaliwa^h

Na mataifa kwa uaminifu
wake.ⁱ

96:9 *Au “Mwabuduni.” #Au labda,
“kwa sababu ya fahari ya utakati-
fu wake.” 96:10 *Au “kutikiswa.” #Au
“Ataamua kesi ya.” 96:13 *Au “ame-
kuja.”

97 Yehova amekuwa
Mfalme!^a
Dunia na iwe na shangwe.^b
Na visiwa vyake vingi
vishangilie.^c

2 Mawingu na giza zito vina-
mzunguka;^d
Uadilifu na haki ndio msi-
ngi wa kiti chake cha
ufalme.^e

3 Moto hutangulia mbele
zake^f
Na kuwateketeza kabisa
maadui wake pande
zote.^g

4 Umeme wake wa radi
huiangazia nchi;
Dunia huona na kute-
temeka.^h

5 Milima huyeyuka kama
nta mbele za Yehova,ⁱ
Mbele za Bwana wa dunia
yote.

6 Mbingu hutangaza uadili-
fu wake,
Na mataifa yote huona
utukufu wake.^j

7 Wote wanaoabudu sana-
mu yoyote ya kuchongwa
na waaibishwe,^k
Wale wanaojigamba ku-
husu miungu yao ya
ubatili.^l

Mwinamieni,^{*} enyi miungu
yote.^m

8 Sayuni husikia na kufu-
rahi;ⁿ
Miji ya Yuda ina^{*} shangwe
Kwa sababu ya hukumu
zako, Ee Yehova.^o

9 Kwa maana wewe, Ee Ye-
hova, ndiye Uliye Juu
Zaidi, juu ya dunia yote;
Umekwezwa juu zaidi ya
miungu mingine yote.^p

97:7 *Au "Mwabuduni." 97:8 *Tnn.,
"Mabinti wa Yuda wana."

SURA YA 97

a Zb 96:10

Ufu 11:16, 17

Ufu 19:6

b Isa 49:13

c Isa 60:9

d Kut 20:21

e Zb 99:4

f Zb 50:3

Da 7:9, 10

g Nah 1:2, 6

Mal 4:1

h Kut 19:16, 18

Zb 77:18

Zb 104:32

i Amu 5:5

Nah 1:5

Hab 3:6

j Hab 2:14

k Yer 10:14

l Isa 37:19

m Kut 12:12

Kut 18:11

n Isa 51:3

o Zb 48:11

p Kut 18:11

Isa 44:8

Safu ya 2

a Zb 34:14

Zb 101:3

Zb 119:104

Ro 12:9

Ebr 1:9

b Zb 37:28

Zb 145:20

c Da 3:28

Mt 6:13

d Zb 112:4

Met 4:18

Isa 30:26

Mik 7:9

SURA YA 98

e Zb 33:3

Zb 96:1

Zb 149:1

Isa 42:10

f Kut 15:11

Zb 111:2

g Kut 15:6

Isa 52:10

Isa 59:16

Isa 63:5

h Lu 2:30, 31

i Isa 5:16

j Law 26:42

Lu 1:54, 55

k Isa 49:6

Mdo 28:28

Ro 10:18

l Zb 47:1

Zb 67:4

10 Enyi mnaompenda Yeho-
va, chukieni maovu.^a
Anaulinda uhai wa^{*} washi-
kamanifu wake;^b

Huwaokoa kutoka katika
mkono wa^m mwovu.^c

11 Nuru imemwangazia mwa-
dilifu^d
Na shangwe walio wanyoo-
fu moyoni.

12 Shangilieni kwa sababu ya
Yehova, enyi waadilifu,
Na mlishukuru jina lake
takatifu.^{*}

Muziki.

98 Mwimbieni Yehova
wimbo mpya,^e

Kwa maana ametenda
mambo yanayostaaja-
bisha.^f

Mkono wake wa kuume,
mkono wake mtakatifu,
umeleta wokovu.^{*g}

2 Yehova ameutangaza
wokovu wake;^h

Amefunua uadilifu wake
mbele ya mataifa.ⁱ

3 Amekumbuka upendo
wake mshikamanifu na
uaminifu wake kwa nyu-
mba ya Israeli.^j

Miisho yote ya dunia imeo-
na wokovu kutoka kwa^{*}
Mungu wetu.^k

4 Mpazieni Yehova sauti ya
ushindi, dunia yote.

Changamkeni na kupaza
sauti kwa shangwe na
kuimba sifa.^{*l}

5 Mwimbieni sifa^{*} Yehova
kwa kinubi,

97:10 *Au "nafsi za." #Tnn., "nguvu
za." 97:12 *Tnn., "muushukuru uku-
mbusho wake." 98:1 *Au "umemle-
tea ushindi." 98:3 *Au "ushindi wa."
98:4 *Au "kupiga muziki." 98:5 *Au
"Mpigieni muziki."

Kwa kinubi na wimbo mtamu.

- 6 Kwa tarumbeta na mlio wa pembe,^a
Pazeni sauti kwa ushindi mbele za Mfalme, Yehova.
- 7 Bahari na ingurume na vitu vyote vinavyojaza, Dunia na wote wanaokaa humo.
- 8 Mito na ipige makofi; Milima na ipaze sauti pamoja kwa shangwe^b
- 9 Mbele za Yehova, kwa maana anakuja* kuihukumu dunia.
Ataihukumu kwa uadilifu dunia inayokaliwa^c
Na mataifa kwa haki.^d
- 99** Yehova amekuwa Mfalme.^e Mataifa na yatetemeke.
Anaketi kwenye kiti cha ufalme juu ya* makerubi.^f Dunia na itikisike.
- 2 Yehova ni mkuu Sayuni, Naye yuko juu ya mataifa yote.^g
- 3 Na walisifu jina lako kuu,^h
Kwa maana linaogopesha, nalo ni takatifu.
- 4 Yeye ni mfalme hodari anayependa haki.ⁱ
Umeimarisha kabisa mambo manyoofu.
Umetekeleza haki na uadilifu^j katika Yakobo.
- 5 Mkwezeni Yehova Mungu wetu^k na kuinama chini* mbele ya kiti cha miguu yake;^l
Yeye ni mtakatifu.^m
- 6 Musa na Haruni walikuwa miongoni mwa makuhani wake,ⁿ

98:9 *Au "amekuja." 99:1 *Au labda, "katikati ya." 99:5 *Au "kuabudu."

SURA YA 98

a Hes 10:10
1Nya 15:28
2Nya 29:27

b Isa 44:23

c Zb 9:8
Mdo 17:31

d Zb 67:4
Zb 96:10
Ro 2:6

SURA YA 99

e Zb 93:1
Ufu 11:17

f Kut 25:22

g Zb 83:18

h Zb 8:1
Zb 148:13
Ufu 15:4

i Ayu 36:6

j Kum 10:17, 18
Yer 9:24

k Kut 15:2

l 1Nya 28:2
Zb 132:7

m Law 19:2

n Kut 24:6
Hes 14:19, 20

Safu ya 2

a 1Sa 7:9

b Kut 15:24, 25
1Sa 15:10

c Kut 19:9

d Kut 40:16
1Sa 12:3

e Kum 9:19

f Mik 7:18

g Kut 34:6, 7

h Kut 15:2

i Zb 2:6

j 1Sa 2:2
Isa 6:3

SURA YA 100

k Zb 95:1, 2
Zb 98:4

l Kum 12:12
Ne 8:10

m Kum 6:4

n Zb 149:2

o Zb 95:6, 7
Eze 34:31
1Pe 2:25

p Zb 50:23
Zb 66:13
Zb 122:1, 2

q Zb 65:4

Na Samweli alikuwa miongoni mwa wale walioliita jina lake.^a

Walikuwa wakimwita Yehova,

Naye alikuwa akiwajibu.^b

- 7 Alikuwa akiongea nao kutoka katika nguzo ya wingu.^c

Walishika vikumbusho vyake na amri aliyo-wapa.^d

- 8 Ee Yehova Mungu wetu, uliwajibu.^e

Ulikuwa Mungu uliyewasamehe,^f

Lakini uliwaadhibu* kwa sababu ya dhambi wali-zotenda.^g

- 9 Mkwezeni Yehova Mungu wetu^h

Na mwiname chini* mbele ya mlima wake mtakatifu,ⁱ

Kwa maana Yehova Mungu wetu ni mtakatifu.^j

Muziki wa shukrani.

100 Mpazieni Yehova sauti ya ushindi, dunia yote.^k

- 2 Mtumikieni Yehova kwa kushangilia.^l

Njooni mbele zake kwa kelele za shangwe.

- 3 Jueni* kwamba Yehova ni Mungu.^m

Yeye ndiye aliyetuumba, na sisi ni mali yake.ⁿ

Sisi ni watu wake na kondo wa malisho yake.^o

- 4 Ingeni katika malango yake kwa shukrani,^p

Katika nyua zake kwa sifa.^q

99:8 *Tnn., "ulilipiza kisasi." 99:9 *Au "mwabudu." 100:3 *Au "Tambueni."

*Au labda, "hatukujiumba wenyewe."

Mshukuruni yeye; lisifuni jina lake.^a

- 5 Kwa maana Yehova ni mwema;^b

Upendo wake mshikamani-fu unadumu milele, Na uaminifu wake katika vizazi vyote.^c

Muziki wa Daudi.

101 Nitaimba kuhusu upendo mshikamani-fu na haki.

Nitakuambia sifa, * Ee Yehova.

- 2 Nitatenda kwa busara na bila lawama.*

Utanjia lini?

Nitatembea kwa utimilifu wa moyo^d ndani ya nyumba yangu.

- 3 Sitaweka kitu chochote kisichofaa* mbele ya macho yangu.

Ninachukia matendo ya wale wanaokengeuka kutoka kwa jambo lililo sawa;^e

Sitashirikiana nao kamwe.[#]

- 4 Moyo uliopotoka uko mbali nami;

Sitakubali* jambo lililo ovu.

- 5 Yeyote anayemchongea jirani yake kwa siri,^f

Nitamnyamazisha.*

Yeyote aliye na macho ya kiburi na moyo wenye majivuno,

Sitamvumilia.

- 6 Nitawatazama waaminifu wa dunia, Ili wakae nami.

101:1 *Au "Nitakupigia muziki." 101:2 *Au "utimilifu." 101:3 *Au "cha ubatili." #Au "Matendo yao hayashikamani nami." 101:4 *Tnn., "Sitajua." 101:5 *Au "Nitamwangamiza."

SURA YA 100

a Zb 96:2
Ebr 13:15

b Zb 86:5
Lu 18:19

c Kut 34:6, 7
Kum 7:9
Zb 98:3

SURA YA 101

d 1Fa 9:4
Zb 78:70, 72

e Zb 97:10

f Met 20:19

Safu ya 2

a Met 20:8

SURA YA 102

b Zb 61:2
Zb 142:2

c Zb 55:1
Da 9:17

d Kut 2:23

e Zb 27:9
Omb 1:20

f Zb 143:7
Isa 65:24

g Omb 1:13

h Zb 143:4

i Zb 6:6
Zb 38:8

j Ayu 19:20
Met 17:22

Yule anayetembea bila lawama* atanihudumia.

- 7 Hakuna mtu yeyote mdanganyifu atakayekaa katika nyumba yangu, Na hakuna mwongo atakayesimama mbele yangu.*

- 8 Kila asubuhi nitawanyamazisha* waovu wote wa dunia,

Nitawaangamiza waovu wote kutoka katika jiji la Yehova.^a

Sala ya mtu aliyekandamizwa, anapokuwa amekata tamaa* na kummwagia Yehova mahangaiko yake.^b

102 Ee Yehova, sikia sala yangu;^c

Kilio changu cha kuomba msaada na kikufikie.^d

- 2 Usinifiche uso wako nina-pokuwa katika taabu.^e

Nitegee sikio lako;*

Nijibu haraka ninapokuita.^f

- 3 Kwa maana siku zangu zinatoweka kama moshi, Na mifupa yangu imeungua na kuwa myeusi kama tanuru.^g

- 4 Moyo wangu umepigwa kama majani na ume-nyauka,^h

Kwa maana ninasahau kula chakula changu.

- 5 Kwa sababu ya kilio changu kikubwa cha maumivu,ⁱ

Mifupa yangu inashikamana na nyama yangu.^j

- 6 Mimi ni kama mwari wa nyikani;

101:6 *Au "kwa utimilifu." 101:7 *Tnn., "mbele ya macho yangu." 101:8 *Au "nitawaangamiza." 102:Uta *Au "anapokuwa dhaifu." 102:2 *Au "Inama chini na unisikilize."

- Mimi ni kama bundi mdo-
go katikati ya magofu.
- 7** Nikilala sipati usingizi;*
Mimi ni kama ndege aliye
peke yake juu ya paa.^a
- 8** Mchana kutwa maadui
wangu wananidhihaki.^b
Wale wanaonidhihaki* wa-
natumia jina langu kama
laana.
- 9** Kwa maana ninakula maji-
vu kama mkate,^c
Na kinywaji changu
kimechanganyika na
machozi,^d
- 10** Kwa sababu ya hasira
yako na ghadhabu yako,
Kwa maana uliniinua juu
ili unitupe tu pembeni.
- 11** Siku zangu zinafifia kama
kivuli,^{*e}
Nami ninanyauka kama
majani.^f
- 12** Lakini wewe unadumu
milele, Ee Yehova,^g
Na umaarufu wako utadu-
mu* katika vizazi vyote.^h
- 13** Kwa hakika utainuka na
kulionyesha rehema
Sayuni,ⁱ
Kwa maana ni wakati
wa kulionyesha kibali
chako;^j
Wakati uliowekwa umefi-
ka.^k
- 14** Kwa maana watumishi
wako wanayathamini
mawe yake^l
Nao wanayapenda hata
mavumbi yake.^m
- 15** Mataifa yataliogopa jina la
Yehova,

102:7 *Au labda, "Nimekonda sana."

102:8 *Au "wanaonifanya nionekane mpumbavu." 102:11 *Au "ni kama ki-
vuli kinachorefuka." 102:12 *Au "jina
lako litadumu." Tnn., "ukumbusho wako
utadumu."

SURA YA 102

a Zb 38:11

b Zb 31:11
Zb 74:10
Zb 79:4

c Omb 3:15

d Zb 80:5

e Zb 39:5

f Ayu 14:1, 2
Zb 102:4

g Zb 90:2

h Kut 3:15

i Isa 49:15

j Isa 60:10

k Ezz 1:1, 2
Isa 40:2
Da 9:2

l Ne 2:3
Zb 137:5

m Zb 79:1

Safu ya 2

a Isa 60:3
Zek 8:22

b Zb 147:2
Yer 33:7

c Isa 60:1

d Da 9:20, 21

e Zb 22:24

f Zb 78:4
Ro 15:4

g 2Nya 16:9

h Kut 3:7
Isa 61:1

i 2Nya 33:12, 13
Zb 79:11

j Zb 9:13, 14
Zb 22:22
Isa 51:11

k Isa 11:10
Isa 49:22
Isa 60:3

l Zb 90:2
Hab 1:12
Ufu 1:8

m Zb 8:3
Isa 48:13
Ebr 1:10-12

Na wafalme wote wa dunia
utukufu wako.^a

- 16** Kwa maana Yehova atalije-
nga upya Sayuni;^b

Atatokea katika utukufu
wake.^c

- 17** Ataisikiliza sala ya ma-
skini;^d

Hataidharau sala yao.^e

- 18** Hili limeandikwa kwa ajili
ya kizazi cha wakati
ujao,^f

Ili watu watakaozaliwa*
baadaye wamsifu Yah.

- 19** Kwa maana yeye hutaza-
ma chini kutoka katika
makao yake matakatifu
yaliyo juu,^g

Kutoka mbinguni Yehova
huitazama dunia,

- 20** Ili asikie kilio cha maumi-
vu cha mfungwa,^h

Ili awaweke huru wale
waliohukumwa kifo,ⁱ

- 21** Ili jina la Yehova litanga-
zwe Sayuni^j

Na sifa yake Yerusalemu,

- 22** Mataifa na falme

Zinapokusanyika pamoja
ili kumtumikia Yehova.^k

- 23** Alininyang'anya nguvu
zangu kabla ya wakati;
Alifupisha siku zangu.

- 24** Nikasema: "Ee Mungu
wangu,

Usiniangamize nikiwa kati-
kati ya maisha yangu,
Wewe ambaye miaka yako
inadumu katika vizazi
vyote.^l

- 25** Zamani za kale uliweka
misingi ya dunia,
Na mbingu ni kazi ya miko-
no yako.^m

- 26** Zitaangamia, lakini wewe
utadumu;

102:18 *Tnn., "watakaumbwa."

Zote zitachakaa kama vazi.

Na kama nguo utazibadili, nazo zitatokomea.

27 Lakini wewe ni yuleyule, na miaka yako haitaisha kamwe.^a

28 Watoto wa watumishi wako watakaa kwa usalama,

Na uzao wao utaimarishwa kabisa mbele zako.”^b

Wa Daudi.

103 Nafsi yangu na imsi-fu Yehova;

Kila kitu kilicho ndani yangu na kilisifu jina lake takatifu.

2 Nafsi yangu na imsi-fu Yehova;

Nami nisisahau kamwe mambo yote aliyotenda.^c

3 Husamehe makosa yako yote^d

Na kuyaponya magonjwa yako yote;^e

4 Huukomboha uhai wako kutoka shimoni.^f

Na kukuvika taji la upendo wake mshikamanifu na rehema.^g

5 Hukushibisha kwa vitu vyema^h maisha yako yote,

Hivi kwamba ujana wako unarudishwa upya kama ule wa tai.ⁱ

6 Yehova hutenda kwa uadilifu/ na haki

Kwa ajili ya wote wanaokandamizwa.^k

7 Alimjulisha Musa njia zake,^l

Na wana wa Israeli mate-ndono yake.^m

103:4 *Au “kaburini.”

SURA YA 102

a Ayu 36:26

Mal 3:6

Yak 1:17

b Isa 66:22

SURA YA 103

c Kum 8:2

Zb 105:5

d 2Sa 12:13

Isa 43:25

e Kut 15:26

Zb 41:3

Zb 147:3

Isa 33:24

Yak 5:15

Ufu 21:4

f Zb 56:13

g Mik 7:18

h Zb 23:5

Zb 65:4

i Zb 51:12

Isa 40:31

j Zb 9:8

k Zb 12:5

Met 22:22, 23

Yak 5:4

l Kut 24:4

Hes 12:8

m Zb 147:19

Safu ya 2

a Isa 55:7

Yak 5:11

b Kut 34:6

Yoe 2:13

Yon 4:2

c Zb 30:5

d Isa 57:16

e Ne 9:31

f Ezr 9:13

Zb 130:3

Isa 55:7

g Zb 103:17

Isa 55:9

h Law 16:21, 22

Isa 43:25

Yer 31:34

i Zb 78:38

Isa 49:15

Mal 3:17

Yak 5:15

j Zb 78:39

k Mwa 2:7

l Zb 90:5, 6

1Pe 1:24

m Ayu 14:1, 2

8 Yehova ni mwenye rehema na mwenye huruma,^{*a}

Si mwepesi wa hasira naye ana upendo mwingi mshikamanifu.^{#b}

9 Hatatafuta makosa siku-zote.^c

Wala hataendelea kuwa na hasira milele.^d

10 Hajatutendea kulingana na dhambi zetu,^e

Wala hajatupa adhabu tuliyostahili kulingana na makosa yetu.^f

11 Kwa maana kama mbingu zilivyo juu kuliko dunia,

Ndivyo upendo wake mshikamanifu ulivyo mkubwa kuelekea wale wanaomwogopa.^g

12 Kama mashariki ilivyo mbali sana na magharibi,

Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali sana na sisi.^h

13 Kama baba anavyowao-nyesha wanawe rehema,

Ndivyo ambavyo Yehova amewaonyesha rehema wale wanaomwogopa.ⁱ

14 Kwa maana anajua vema umbo letu,^j

Akikumbuka kwamba sisi ni mavumbi.^k

15 Siku za mwanadamu anayeweza kufa ni kama za majani;^l

Yeye huchanua kama ua la shambani.^m

16 Lakini upepo unapovuma, linatoweka,

Kana kwamba halikuwahi kuwepo.*

103:8 *Au “neema.” #Au “fadhili nyingi zenye upendo.” 103:16 *Tnn., “Na mahali pake hapalijui tena.”

17 Lakini upendo mshikamafu wa Yehova ni wa milele na milele*
Kuelekea wale wanaomwogopa,^a
Na uadilifu wake kuelekea watoto wa watoto wao,^b

18 Kuelekea wale wanaolishika agano lake^c
Na wale walio waangalifu ili kuyashika maagizo yake.

19 Yehova amekiimarisha kabisa kiti chake cha ufalme mbinguni,^d
Nao ufalme wake unatawala kila kitu.^e

20 Msifuni Yehova, enyi malaika wake wote,^f mlio na nguvu nyingi,
Mnaotekeleza neno lake,^g mkitii sauti yake.*

21 Msifuni Yehova, enyi majeshi yake yote,^h
Ninyi wahudumu wake mnaofanya mapenzi yake.ⁱ

22 Msifuni Yehova, kazi zake zote,
Kila mahali anapotawala.*
Nafsi yangu yote na imsifu Yehova.

104 Nafsi yangu na imsifu Yehova.^j
Ee Yehova Mungu wangu, wewe ni mkuu sana.^k
Umevaa utukufu* na fahari.^l

2 Umejifunika nuru^m kama vazi;
Unazitandaza mbingu kama kitambaa cha hema.ⁿ

103:17 *Au "tangu milele hadi milele."
103:20 *Tnn., "mkiisikia sauti ya neno lake."
103:22 *Au "Kila mahali pa enzi yake kuu."
104:1 *Au "adhama."

SURA YA 103

a Lu 1:50

b Kut 20:6

c Kut 19:5
Kum 7:9
Zb 25:10d 2Nya 20:6
Isa 66:1e Zb 47:2
Zb 145:13
Da 4:25

f Da 7:10

g 2Fa 19:35
Lu 1:19h 1Fa 22:19
Zb 148:2
Lu 2:13, 14i Mt 13:41
Ebr 1:7

SURA YA 104

j Zb 103:1

k Zb 86:10

l 1Nya 16:27
Eze 1:27, 28
Da 7:9m Yak 1:17
1Yo 1:5

n Isa 40:22

Safu ya 2

a Zb 18:11
Amo 9:6b Kum 33:26
Isa 19:1c 2Sa 22:11
Ayu 38:1d Eze 1:13
Ebr 1:7, 14e Ayu 38:4, 6
Zb 24:1, 2

f Mhu 1:4

g Mwa 1:2

h Mwa 1:9

i Met 8:25

j Ayu 38:8-10
Zb 33:7
Met 8:29
Yer 5:22

3 Hujenga boriti za vyumba vyake vya juu katika maji yaliyo juu,^a

Akiyafanya mawingu kuwa gari lake,^b
Akienda juu ya mabawa ya upepo.^c

4 Huwafanya malaika wake kuwa roho,
Wahudumu wake kuwa moto unaoteketeza kabisa.^d

5 Ameiimarisha dunia juu ya misingi yake;^e
Haitasogezwa kutoka mahali pake* milele na milele.^f

6 Uliifunika kwa vilindi vya maji kama kwa vazi.^g
Maji yalisimama juu ya milima.

7 Kwa kimeo lako yalikiambia;^h
Kwa sauti ya mngurumo wako yalikingia kwa wasiwasi

8 —Milima ilipandaⁱ na mabonde yakashuka—
Mahali ulipokusudia yawepo.

9 Uliweka mpaka ambao hayapaswi kuvuka,^j
Ili yasiifunike dunia tena kamwe.

10 Wewe hupeleka chemchemi katika mabonde;*
Kati ya milima zinatiririka.

11 Zinawapa maji wanyama wote wa mwituni;
Punda mwitu hukata kiu yake.

12 Juu yake ndege wa angani hukaa;
Wanaimba katikati ya majani mengi.

104:3 *Tnn., "katika maji." 104:5 *Au "Haitatikiswa." 104:10 *Au "makorongu."

- 13** Anainyvesha milima maji kutoka katika vyumba vyake vya juu.^a
Dunia hushibishwa kwa matunda ya kazi zako.^b
- 14** Anaotesha majani kwa ajili ya ng'ombe
Na mimea kwa ajili ya matumizi ya wanadamu,^c
Ili chakula kikue ardhini
- 15** Na divai inayofanya moyo wa mwanadamu ushangelie,^d
Mafuta yanayofanya uso ungu'ae,
Na mkate unaotegemeza moyo wa mwanadamu anayeweza kufa.^e
- 16** Miti ya Yehova imetosheka,
Mierezi ya Lebanoni aliyo-panda,
- 17** Ambamo ndege hutenge-neza viota.
Makao ya korongo^f ni miberoshi.
- 18** Milima mirefu ni ya mbuzi wa milimani;^g
Majabali ni kimbilio la wibari.^h
- 19** Ameuumba mwezi ili upime nyakati zilizowekwa;
Jua linajua vizuri wakati wa kutua.ⁱ
- 20** Wewe unaleta giza, usiku unaingia,^j
Wakati ambapo wanyama wote wa mwituni wanazunguka-zunguka.
- 21** Wanasimba* hunguruma ili wapate mawindo^k
Na kutafuta chakula chao kutoka kwa Mungu.^l
- 22** Jua linapocho moja, Wanarudi na kulala katika mapango yao.

104:21 *Au "Wanasimba wenye manyoya marefu shingoni."

SURA YA 104

a Ayu 38:37
Zb 147:8
Yer 10:13
Amo 9:6
Mt 5:45

b Zb 65:9
Mdo 14:17

c Mwa 1:29, 30
Mwa 9:3

d Mhu 9:7

e Mhu 10:19

f Yer 8:7

g Ayu 39:1

h Met 30:26

i Mwa 1:16
Zb 19:6
Yer 31:35

j Mwa 1:5
Zb 74:16
Isa 45:7

k Amo 3:4

l Zb 147:9

Safu ya 2

a Ne 9:6

b Met 3:19
Yer 10:12

c Mwa 1:21

d Ayu 41:1

e Zb 136:25
Zb 145:15
Zb 147:9
Mt 6:26

f Lu 12:24

g Zb 107:9
Zb 145:16

h Mwa 3:19
Ayu 34:14, 15
Zb 146:3, 4
Mhu 3:19, 20
Mhu 12:7

i Ayu 33:4
Mdo 17:28

j Mwa 1:31

k Kut 19:18

l Zb 13:6

- 23** Mwanadamu huenda kwenye kazi yake,
Naye hufanya kazi kwa jasho mpaka jioni.
- 24** Jinsi kazi zako zilivyo nyingi sana, Ee Yehova!^a
Umezifanya zote kwa hekima.^b
Dunia imejaa vitu ulivyo-umba.
- 25** Kisha kuna bahari, ni kubwa sana na pana,
Imejaa viumbe walio hai wasio na idadi, wadogo kwa wakubwa.^c
- 26** Humo meli husafiri,
Na Lewiathani,^{*d} uliyemuumba ili acheze humo.
- 27** Wote wanakungojea wewe Uwape chakula chao kwa wakati wake.^e
- 28** Wanakusanya unachowapa.^f
Unapofumbua mkono wako, wanashiba vitu vyema.^g
- 29** Ukiuficha uso wako, wanahangaika.
Ukiiondoa roho yao, wanakufa na kurudi mavumbini.^h
- 30** Ukiituma roho yako, wanaumbwa,ⁱ
Nawe unaifanya ardhi iwe na sura mpya.
- 31** Utukufu wa Yehova utadumu milele.
Yehova atashangilia kwa sababu ya kazi zake.^j
- 32** Huitazama dunia, inatetemeka;
Huigusa milima, inafuka moshi.^k
- 33** Nitamwambia Yehova' mai-sha yangu yote;

104:26 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

Nitamwimbia sifa* Mungu wangu maadamu nina-ishi.^a

34 Mawazo yangu na yampe-ndeze.*

Nitashangilia kwa sababu ya Yehova.

35 Watenda dhambi watato-weka duniani, Na waovu hawatakuwapo tena.^b

Nafsi yangu na imsifu Yehova. Msifuni Yah!*

105 Mshukuruni Yehova,^c liitieni jina lake,

Yajulisheni mataifa mate-ndo yake!^d

2 Mwimbieni, mwimbieni sifa,*

Tafakarini[#] kazi zake zote zinazostaajibisha.^e

3 Jivunieni jina lake taka-tifu.^f

Mioyo ya wale wanao-mtafuta Yehova na ishangilie.^g

4 Mtafuteni Yehova^h na ngu-vu zake.

Utafuteni uso* wake daima.

5 Kumbukeni kazi zinazo-staajibisha alizofanya, Miujiza yake na hukumu alizotangaza,ⁱ

6 Enyi uzao wa* Abrahamu mtumishi wake,^j

Enyi wana wa Yakobo, watu wake aliowa-chagua.^k

104:33 *Au "Nitampigia muziki."

104:34 *Au labda, "Kutafakari kwangu kumhusu na kupendeze." **104:35** *Au "Haleluya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova. **105:2** *Au "mpigieni muziki."[#] Au labda, "Zungumzieni." **105:4** *Au "uwepo." **105:6** *Au "wazao wa." Tnn., "mbegu ya."

SURA YA 104

a Zb 146:2

b Zb 37:10, 38
Met 2:22

SURA YA 105

c Zb 136:1

d 1Nya 16:8-13
Zb 96:3
Zb 145:11, 12
Isa 12:4

e Zb 77:12
Zb 119:27

f Yer 9:24

g Zb 119:2

h Amo 5:4
Sef 2:3

i Kum 7:18, 19

j Kut 3:6

k Kut 19:5, 6
Isa 41:8

Safu ya 2

a Kut 20:2
Zb 100:3

b 1Nya 16:14-18
Isa 26:9
Ufu 15:4

c Ne 1:5

d Kum 7:9
Lu 1:72, 73

e Mwa 17:1, 2
Mwa 22:15-18

f Mwa 26:3

g Mwa 12:7
Mwa 13:14, 15
Mwa 15:18
Mwa 26:3
Mwa 28:13

h Zb 78:55

i Mwa 34:30

j Mwa 17:8
Mwa 23:4
1Nya 16:19-22
Mdo 7:4, 5

k Mwa 20:1
Mwa 46:6

l Mwa 31:7, 42

m Mwa 12:17
Mwa 20:2, 3

n Mwa 26:9, 11

o Mwa 41:30, 54
Mwa 42:5
Mdo 7:11

7 Yeye ni Yehova Mungu wetu.^a

Hukumu zake ziko duniani kote.^b

8 Anakumbuka agano lake milele,^c

Ahadi aliyotoa,* hata kufikia vizazi elfu,^d

9 Agano alilofanya na Abrahamu,^e

Na kiapo alichomwapia Isaka,^f

10 Alichotoa kama amri kwa Yakobo

Na kama agano la kudumu kwa Israeli,

11 Akisema, "Nitakupa nchi ya Kanaani^g

Kuwa urithi wako ulioga-wiwa."^h

12 Wakati walipokuwa wachache,ⁱ

Naam, wachache sana, nao walikuwa wageni nchini.^j

13 Walitembea kutoka taifa moja hadi taifa lingine,

Kutoka ufalme mmoja hadi ufalme mwingine.^k

14 Hakumruhusu mtu yeyote awakandamize,^l

Lakini kwa sababu yao aliwakaripia wafalme,^m

15 Akisema, "Msiwaguse watiwa-mafuta wangu, Wala msiwatendee manabii wangu jambo lolote baya."ⁿ

16 Alileta njaa kali nchini;^o Alifanya wakose mikate.*

17 Alimtuma mtu awatanguilie

105:8 *Tnn., "Neno aliloamuru."

105:16 *Tnn., "Aliuvunja kila ufito wa mikate." Labda ni fito zilizotumiwa kuhifadhi mikate.

Ambaye aliuzwa kuwa mtumwa, Yosefu.^a

- 18** Waliifunga* miguu yake kwa pingu,^b Shingo yake ilitiwa katika vyuma;[#]
- 19** Mpaka wakati ambapo neno lake lilitimia,^c Neno la Yehova ndilo lililomsafisha.
- 20** Mfalme aliamuru afungu-liwe,^d Mtawala wa mataifa akamweka huru.
- 21** Akamweka kuwa bwana mkubwa wa nyumba yake, Mtawala wa mali zake zote,^e
- 22** Ili awe na mamlaka juu ya* wakuu wake kama alivyopenda[#] Na kuwafundisha wazee wake hekima.^f
- 23** Kisha Israeli akaja Misri,^g Na Yakobo akakaa akiwa mgeni katika nchi ya Hamu.
- 24** Mungu aliwafanya watu wake waongezeke sana;^h Aliwafanya wawe na nguvu kuliko maadui wao,ⁱ
- 25** Akaruhusu mioyo yao ibadilike ili wawachukie watu wake, Ili wapange njama dhidi ya watumishi wake.^j
- 26** Alimtuma Musa mtumishi wake,^k Na Haruni,^l aliyekuwa amemchagua.
- 27** Walifanya ishara zake kati yao,

105:18 *Tnn., "Waliitesa." #Au "Nafsi yake iliingia katika chuma." 105:22 *Tnn., "Ili awafunge." #Au "kama nafsi ilivyotaka."

SURA YA 105

a Mwa 37:28, 36
Mwa 45:4, 5
Mwa 50:20

b Mwa 39:20

c Mdo 7:10

d Mwa 41:14

e Mwa 41:39-41
Mwa 41:48
Mwa 45:8

f Mwa 41:33, 38

g Mwa 46:4, 6

h Kut 1:7
Mdo 7:17

i Kut 1:8, 9

j Kut 1:10
Mdo 7:18, 19

k Kut 3:10
Kut 4:12
Kut 6:11

l Kut 4:14
Kut 7:1

Safu ya 2

a Ne 9:10
Zb 78:43-51

b Kut 10:22, 23

c Kut 7:20, 21

d Kut 8:6

e Kut 8:17, 24

f Kut 9:23-26

g Kut 10:13-15

h Kut 12:29

i Mwa 15:13, 14
Kut 3:22
Kut 12:35, 36

Miujiza yake katika nchi ya Hamu.^a

- 28** Alilituma giza na nchi ikawa giza;^b Hawakuasi maneno yake.
- 29** Alibadili maji yao yakawa damu Na kuwaua samaki wao.^c
- 30** Nchi yao ikajaa vyura,^d Hata katika vyumba vya mfalme.
- 31** Aliagiza nzi wavamie Na mbu* katika maeneo yao yote.^e
- 32** Aliibadili mvua yao ikawa mvua ya mawe Naye akatuma radi* katika nchi yao.^f
- 33** Aliipiga mizabibu yao na mitini yao Na kuivunjavunja miti ya eneo lao.
- 34** Aliagiza nzige wavamie, Nzige wachanga wasio na idadi.^g
- 35** Walikula kabisa mimea yote nchini, Nao wakala kabisa mazao ya ardhi.
- 36** Kisha akamuua kila mzaliwa wa kwanza katika nchi yao,^h Mwanzo wa nguvu zao za uzazi.
- 37** Aliwatoa nje watu wake wakiwa na fedha na dhababu;ⁱ Na hakuna yeyote katika makabila yake aliyeki-kwaa.
- 38** Misri ilishangilia walipoondoka, Kwa maana hofu ya

105:31 *Aina ya mbu anayelitwa *hakkin-nam'* katika Kiebrania. 105:32 *Au "miali ya moto."

Israeli* ilikuwa imewa-shika.^a

39 Alitandaza wingu ili liwa-funike^b

Na moto uangaze wakati wa usiku.^c

40 Waliomba, naye akaleta kware;^d

Aliendelea kuwashibisha mkate kutoka mbinguni.^e

41 Alifungua mwamba, maji yakatiririka kutoka humo;^f

Maji hayo yalitiririka jangwani kama mto.^g

42 Kwa maana aliikumbuka ahadi takatifu aliyompa Abrahamu mtumishi wake.^h

43 Kwa hiyo akawatoa watu wake wakishangilia,ⁱ Watu wake aliowachagua aliwatoa kwa kilio cha shangwe.

44 Aliwapa nchi za mataifa;^j Walirithi vitu ambavyo mataifa mengine yalikuwa yametaabika kuvipata,^k

45 Ili waweze kutii maagizo yake^l

Na kushika sheria zake. Msifuni Yah!*

106 Msifuni Yah!* Mshukuruni Yehova, kwa maana yeye ni mwema;^m

Upendo wake mshikamani-fu unadumu milele.ⁿ

2 Ni nani anayeweza kutangaza kikamili matendo ya Yehova yenye nguvu

105:38 *Tnn., "hofu yao." 105:45; 106:1 *Au "Haleluya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova.

SURA YA 105

a Kut 12:33

b Kut 14:19, 20

c Kut 13:21

d Zb 78:27

e Kut 16:12-15
Zb 78:24

f Kut 17:6
1Ko 10:1, 4

g Zb 78:15, 16

h Mwa 12:7
Mwa 15:13, 14
Kut 2:24
Kum 9:5

i Hes 33:3

j Yos 11:23
Yos 21:43
Ne 9:22
Zb 78:55
Mdo 13:19

k Kum 6:10, 11
Yos 5:11, 12

l Kum 4:40

SURA YA 106

m Lu 18:19

n 1Nya 16:34
Ezr 3:11
Zb 103:17
Zb 107:1

Safu ya 2

a Zb 40:5

b Zb 15:1, 2
Isa 64:5

c Ne 5:19
Zb 51:18
Zb 119:132

d Kut 19:5

e Ne 9:16
Zb 78:8

f Ezr 9:6
Da 9:5

g Kut 14:11, 12

h Zb 143:11
Eze 20:14

i Kut 9:16
Ro 9:17

j Kut 14:21, 22

k Kut 14:30

Au kutangaza matendo yake yote yanayostahili sifa?^a

3 Wenye furaha ni wale wanaotenda haki,

Ambao sikuzote wanatenda yaliyo sawa.^b

4 Nikumbuke, Ee Yehova, unapowaonyesha kibali* watu wako.^c

Nitunze kwa matendo yako ya wokovu,

5 Ili nifurahie wema unapowaonyesha watu wako uliowachagua,^d

Ili nishangilie pamoja na taifa lako,

Ili nikusifu kwa fahari* pamoja na urithi wako.

6 Tumetenda dhambi kama mababu zetu;^e

Tumetenda kosa; tumetenda uovu.^f

7 Mababu zetu kule Misri hawakuthamini* kazi zako zinazostaajibisha.

Hawakukumbuka upendo wako mwingi mshikamani-fu,

Bali waliasi baharini, kando ya Bahari Nyekundu.^g

8 Lakini aliwaokoa kwa ajili ya jina lake,^h

Ili kufanya nguvu zake zijulikane.ⁱ

9 Aliikemea Bahari Nyekundu, ikakauka;

Aliwaongoza katika vilindi vyake kana kwamba wanaipitia jangwani;^{*j}

10 Aliwaokoa kutoka mikono-ni mwa adui yao^k

106:4 *Au "nia njema." 106:5 *Au "nijigambe kukuhusu." 106:7 *Au "hawakuelewa maana ya." 106:9 *Au "nyikani."

- Na kutoka mikononi mwa adui aliwakomboa.^a
- 11** Maji yaliwafunika maadui wao;
Hakuna hata mmoja wao aliyeokoka.^{*b}
- 12** Kisha wakawa na imani katika ahadi yake;^c
Wakaanza kuimba sifa yake.^d
- 13** Lakini walisahau haraka mambo aliyotenda;^e
Hawakungojea ushauri wake.
- 14** Walifuata tamaa zao za kichoyo nyikani;^f
Walimjaribu Mungu jangwani.^g
- 15** Aliwapa walichoomba, Lakini akawapiga kwa ugonjwa uliowadhoo-fisha.^h
- 16** Walimwonea wivu Musa kambini
Na Haruni,ⁱ mtakatifu wa Yehova.^j
- 17** Kisha dunia ikafunguka na kummeza Dathani
Na kuwafunika wale waliokusanyika pamoja na Abiramu.^k
- 18** Moto uliwaka katika kundi lao;
Mwali wa moto ukawateke-teza kabisa waovu.^l
- 19** Walitengeneza ndama kule Horebu
Na kuiinamia sanamu ya chuma;^{*m}
- 20** Waliubadili utukufu wangu
Kwa mfano wa ng'ombe dume anayekula nyasi.ⁿ
- 21** Walimsahau Mungu^o Mwo-kozi wao,

106:11 *Au "aliyebaki." 106:19 *Au "sanamu ya kuyeyushwa."

SURA YA 106

- a Isa 49:26
b Kut 14:13, 28
c Kut 14:31
d Kut 15:1
e Kut 15:24
Kut 16:2, 3
Kut 17:7
f Hes 11:4
Kum 9:22
IKo 10:6
g Kut 17:2
Zb 78:18
IKo 10:9
Ebr 3:8, 9
h Hes 11:31, 33
Zb 78:29-31
i Hes 16:3
j Law 21:8
Hes 16:5-7
k Hes 16:27, 32
l Hes 16:35
m Kut 32:4
Kum 9:12
n Kut 20:4
o Kum 32:18

Safu ya 2

- a Kum 4:34
b Zb 78:51
c Kut 14:25
d Kut 32:10, 11
Kum 9:14, 19
e Hes 13:32
Kum 8:7-9
f Hes 14:11
g Hes 14:2
Kum 1:27
h Hes 14:22, 23
i Hes 14:28, 29
Ebr 3:11
j Law 26:33
Kum 4:27
k Hes 25:3
Ho 9:10
l Hes 25:6
Kum 32:16
m Hes 25:9
IKo 10:8
n Hes 25:7, 8

- Aliyetenda mambo makuu nchini Misri,^a
- 22** Kazi zinazostaajabisha katika nchi ya Hamu,^b
Mambo yanayoogopesha kwenye Bahari Nyekundu.^c
- 23** Alikuwa karibu kuamuru waangamizwe,
Lakini Musa, mchaguliwa wake, akaingilia kati*
Ili kuzuia hasira yake inayoangamiza.^d
- 24** Kisha wakaidharau ile nchi inayotamanika;^e
Hawakuwa na imani katika ahadi yake.^f
- 25** Waliendelea kunung'unika katika mahema yao;^g
Hawakuisikiliza sauti ya Yehova.^h
- 26** Kwa hiyo akainua mkono wake na kuapa kuwahuu
Kwamba angewaangusha nyikani;ⁱ
- 27** Angewaangusha wazao wao miongoni mwa mataifa,
Naye angewatawanya katika nchi mbalimbali.^j
- 28** Kisha wakajiunga* na ibada ya Baali wa Peori,^k
Nao wakala dhabihu zilizo-tolewa kwa waliokufa.[#]
- 29** Walimkasirisha kwa mate-ndo yao,^l
Na pigo likazuka miongoni mwao.^m
- 30** Lakini Finehasi alipoinuka na kuingilia kati,
Pigo hilo lilikomeshwa.ⁿ

106:23 *Tnn., "akasimama kwenye pengo hilo mbele zake." 106:28 *Au "wakashikamana." #Yaani, dhabihu zilizo-tolewa kwa watu waliokufa au kwa miungu ambayo haina uhai.

- 31** Na jambo hilo likahesa-
biwa kwake kuwa
uadilifu
Katika vizazi vyote milele.^a
- 32** Walimkasirisha kwenye
maji ya Meriba,*
Na mambo yakamwendea
Musa vibaya kwa sababu
yao.^b
- 33** Waliitia chungu roho
yake,
Naye akaongea bila kufiki-
ri kwa midomo yake.^c
- 34** Hawakuyaangamiza ma-
taifa,^d
Kama Yehova alivyokuwa
amewaamuru.^e
- 35** Lakini walichangamana
na mataifa hayo^f
Na kuzikubali* njia zao.^g
- 36** Waliendelea kuabudu sa-
namu zao,^h
Nazo zikawa mtego kwao.ⁱ
- 37** Waliwatoa dhabihu
wana wao
Na mabinti wao kwa roho
waovu.^j
- 38** Waliendelea kumwaga
damu isiyo na hatia,^k
Damu ya wana wao na ma-
binti wao wenyewe
Ambao waliwatoa dhabi-
hu kwa sanamu za
Kanaani;^l
Na nchi ikachafuliwa kwa
umwagaji wa damu.
- 39** Wakawa wachafu kwa sa-
babu ya kazi zao;
Walifanya ukahaba wa ki-
roho kwa matendo yao.^m
- 40** Kwa hiyo hasira ya Yehova
ikawaka dhidi ya watu
wake,
Naye akauchukia sana uri-
thi wake.

106:32 *Maana yake "Kugombana."
106:35 *Au "kujifunza."

SURA YA 106

a Hes 25:11-13

b Hes 20:2, 12
Hes 27:13, 14

c Hes 20:10

d Yos 16:10
Yos 17:12
Amu 1:21e Hes 33:52
Kum 7:1, 2f Yos 15:63
Amu 1:33

g Isa 2:6

h Amu 2:11, 12
2Fa 17:12

i Kut 23:32, 33

j Kum 12:31
2Fa 16:1, 3
2Fa 17:17, 18
Yer 7:30, 31
IKo 10:20

k 2Fa 21:16

l Eze 16:20

m Yer 3:9

Safu ya 2

a Kum 32:30
Amu 3:8

b Amu 10:6-8

c Amu 10:11, 12
1Sa 12:11

d Amu 4:1

e Amu 6:1-5

f Amu 2:18

g Amu 3:9

h Kut 34:6
Kum 32:36
Isa 63:7
Omb 3:32
Yoe 2:13

i Eze 9:9

j Zb 79:9

k Yer 32:37

l 1Nya 16:35

m 1Nya 29:10
Zb 41:13
Lu 1:68

- 41** Aliwatia tena na tena mi-
kononi mwa mataifa,^a
Ili wale waliowachukia wa-
weze kuwatawala.^b
- 42** Maadui wao waliwakanda-
miza,
Nao wakatiishwa chini ya
nguvu zao.*
- 43** Aliwaokoa mara nyingi,^c
Lakini walikuwa wakiasi
na kukosa kutii,^d
Nao walikuwa wakifedhe-
heshwa kwa sababu ya
makosa yao.^e
- 44** Lakini alikuwa akiona taa-
bu yao^f
Na kusikia kilio chao cha
kuomba msaada.^g
- 45** Na kwa ajili yao alikuwa
akikumbuka agano lake,
Naye alikuwa akiwahuru-
mia,* akichocheva na
upendo wake mwingi^h
mshikamanifu.^h
- 46** Alikuwa akisababisha wa-
hurumiwe
Na wote waliowachukua
mateka.ⁱ
- 47** Tuokoe, Ee Yehova Mungu
wetu,^j
Na kutukusanya kutoka
katika mataifa^k
Ili tulishukuru jina lako ta-
katifu
Na tushangilie kukusifu
wewe.*^l
- 48** Yehova, Mungu wa Israeli,
na asifiwe
Kwa umilele wote.*^m
Na watu wote waseme,
"Amina!"[#]
Msifuni Yah![△]

106:42 *Tnn., "mkono wao." 106:45
*Au "akighairi." #Au "mkubwa; mkuu."
106:47 *Au "tupate shangwe kwa ku-
kusifu." 106:48 *Au "Milele na milele."
#Au "Na iwe hivyo!" △Au "Haleluya!"
"Yah" ni ufupisho wa jina Yehova.

KITABU CHA TANO
(Zaburi 107-150)

107 Mshukuruni Yehova,
kwa maana yeye ni
mwema;^a

Upendo wake mshikamani-
fu unadumu milele.^b

2 Wale waliokombolewa*
na Yehova na waseme
jambo hilo,

Wale aliowakomboa kuto-
ka mikononi mwa[#] adui,^c

3 Wale aliowakusanya pa-
moja kutoka katika nchi
mbalimbali,^d

Kutoka mashariki na kuto-
ka magharibi,*

Kutoka kaskazini na kuto-
ka kusini.^e

4 Walitangatanga nyikani,
jangwani;

Hawakupata njia ya kwe-
nda katika jiji ambamo
wangeweza kuishi.

5 Walikuwa na njaa na kiu;
Walidhoofika kwa sababu
ya uchovu.

6 Waliendelea kumlilia
Yehova walipokuwa
wakitaabika;^f
Aliwaokoa kutoka katika
dhiki yao.^g

7 Aliwaongoza kutembea
katika njia inayofaa^h
Ili wafike katika jiji amba-
mo wangeweza kuishi.ⁱ

8 Watu na wamshukuru
Yehova/ kwa sababu ya
upendo wake mshikama-
nifu

Na kwa sababu ya kazi
zake zinazostaajibisha
anzawatendea wana-
damu.^k

107:2 *Au "walionunuliwa." #Au "kati-
ka nguvu za." 107:3 *Au "Kutoka ma-
pambazuko ya jua na kutoka machweo
ya jua."

SURA YA 107

a Lu 18:19

b 1Nya 16:34
Zb 103:17c Isa 35:10
Yer 15:21
Mik 4:10d Zb 106:47
Yer 29:14e Isa 43:5, 6
Yer 31:8

f Ho 5:14, 15

g Isa 41:17

h Isa 30:21

i Ne 11:3

j 1Nya 16:8

k Zb 40:5

Safu ya 2

a Zb 34:10
Isa 55:2
Lu 1:53b Zb 106:43
Omb 3:42

c Law 26:21

d Zb 68:6
Zb 146:7
Isa 49:8, 9
Isa 61:1

e Omb 3:22

f Isa 45:1, 2

g Yer 2:19

h Omb 3:39

9 Kwa maana amewatoshe-
leza wenye kiu*
Na kuwashibisha wenye
njaa[#] kwa vitu vyema.^a

10 Baadhi yao walikuwa wa-
kiishi katika giza zito
sana,
Wafungwa walioteseka na
kufungwa kwa vyuma.

11 Kwa maana walikuwa wa-
meliasi neno la Mungu;
Waliudharau ushauri wa
Aliye Juu Zaidi.^b

12 Kwa hiyo aliinyenyekeza
mioyo yao kupitia
taabu;^c

Walijikwaa, na hakukuwa
na yeyote wa kuwasa-
idia.

13 Walimlilia Yehova awa-
saidie walipokuwa
wakitaabika;
Akawaokoa kutoka katika
dhiki yao.

14 Aliwatoa katika giza zito
sana,
Na kuzikata pingu zao.^d

15 Watu na wamshukuru
Yehova kwa sababu ya
upendo wake mshikama-
nifu^e

Na kwa sababu ya kazi
zake zinazostaajibisha
anzawatendea wana-
damu.

16 Kwa maana ameivunja mi-
lango ya shaba
Na kuyakata makomeo ya
chuma.^f

17 Walikuwa wapumbavu,
nao wakateseka^g
Kwa sababu ya makosa
yao na dhambi zao.^h

107:9 *Au "amezitoshesheleza nafsi zilizo-
kauka." #Au "kuzishibisha nafsi zenye
njaa."

- 18** Walipoteza hamu ya kula kila aina ya chakula;* Waliyakaribia malango ya kifo.
- 19** Walikuwa wakimlilia Yehova awasaidie walipokuwa wakitaabika; Naye alikuwa akiwaokoa kutoka katika dhiki yao.
- 20** Alikuwa akituma neno lake na kuwaponya^a Na kuwaokoa kutoka katika mashimo ambamo walikuwa wamenaswa.
- 21** Watu na wamshukuru Yehova kwa sababu ya upendo wake mshikamanifu Na kwa sababu ya kazi zake zinazostaajibisha anazawatendea wadamu.
- 22** Na watoe dhabihu za shukrani^b Na kutangaza kazi zake kwa kilio cha shangwe.
- 23** Wale wanaosafiri kwa meli baharini, Wanaofanya biashara yao kwenye maji mengi,^c
- 24** Wameziona kazi za Yehova Na kazi zake zinazostaajibisha zilizo vilindini;^d
- 25** Jinsi dhoruba ya upepo inavyoinuka kwa neno lake,^e Na kuyainua mawimbi ya bahari.
- 26** Hayo huinuka juu angani; Hushuka chini kwa nguvu vilindini. Ujasiri wao* huyeyuka kwa sababu ya msiba unaokaribia.
- 27** Wao hugaagaa na kupepesuka kama mlevi,

107:18 *Au "Walichukia kabisa vyakula vyote." 107:26 *Au "Nafsi yao."

SURA YA 107

a Zb 147:3

b Law 7:12
Zb 50:14

c 2Nya 9:21
Eze 27:9

d Mwa 1:21
Zb 104:25

e Zb 135:7
Yer 10:13
Yon 1:4

Safu ya 2

a Yon 1:4, 13

b Yon 1:14

c Zb 65:7
Zb 89:9
Yon 1:15

d Zb 105:5

e Zb 111:1

f 1Fa 17:1, 7
Isa 42:15
Amo 4:7

g Mwa 13:10
Kum 29:22, 23

h 2Fa 3:17
Isa 35:7
Isa 41:18

i Zb 146:7
Lu 1:53

j Zb 107:7

- Na ustadi wao wote unakosa manufaa kabisa.^a
- 28** Kisha wanamlilia Yehova kwa sauti wanapotaabika,^b Naye huwaokoa kutoka katika dhiki yao.
- 29** Yeye huituliza dhoruba ya upepo; Mawimbi ya bahari hunyamaza.^c
- 30** Wanashangilia yanapotulia, Naye huwaongoza kwenda kwenye bandari wanayotamani.
- 31** Watu na wamshukuru Yehova kwa sababu ya upendo wake mshikamanifu Na kwa sababu ya kazi zake zinazostaajibisha anazawatendea wadamu.^d
- 32** Na wamkweze katika kutaniko la watu,^e Na wamsifu katika baraza la* wazee.
- 33** Yeye hubadili mito kuwa jangwa, Na chemchemi za maji kuwa ardhi iliyokauka,^f
- 34** Nchi inayozaa kuwa nchi iliyoharibika yenye chumvi,^g Kwa sababu ya uovu wa wale wanaokaa humo.
- 35** Yeye hulibadili jangwa kuwa madimbwi ya maji yenye matete, Na nchi kavu kuwa chemchemi za maji.^h
- 36** Huwafanya wenye njaa wakae humo,ⁱ Ili wajenge jiji ambamo wanaweza kuishi.^j

107:32 *Tnn., "kwenye kiti cha."

37 Wanapanda mbegu mashambani na kupanda mashamba ya mizabibu^a Yanayozaa mazao mengi.^b

38 Huwabariki, nao huongezeka sana; Haachi ng'ombe wao wapungue.^c

39 Kisha wanakuwa wachache tena na kuaibishwa Kwa sababu ya ukandamizaji, msiba, na huzuni.

40 Huwamwagia wakuu dharau Na kuwafanya watangeta-nge jangwani kusiko na njia.^d

41 Lakini huwalinda* maskini ili wasikandamizwe^e Na kufanya familia zao ziwe nyingi kama kundi la kondoo.

42 Wanyoofu huona hilo na kushangilia;^f Lakini vaovu wote hufunga vinywa vyao.^g

43 Yeyote aliye na hekima atayachunguza mambo hayo^h Naye atatafakari kwa makini matendo ya Yehova ya upendo mshikamanifu.ⁱ

Wimbo. Muziki wa Daudi.

108 Moyo wangu uko imara, Ee Mungu. Nitaimba na kupiga muziki kwa nafsi yangu yote.*^j

2 Amka, Ee kinanda; nawe pia, Ee kinubi.^k Nitayaamsha mapambazuko.

3 Nitakusifu miongoni mwa mataifa, Ee Yehova,

107:41 *Au "huwainua juu," yaani, ili wasifikwiwe. 108:1 *Tnn., "hata kwa utukufu wangu."

SURA YA 107

a Isa 65:21

b Mdo 14:17

c Kum 7:13, 14

d Ayu 12:21, 24

e 1Sa 2:8

f Zb 58:10

g Kut 11:7
Zb 63:11

h Zb 64:9
Ho 14:9

i Zb 77:12
Zb 143:5
Yer 9:24

SURA YA 108

j Zb 57:7-11
Zb 104:33

k Zb 81:2

Safu ya 2

a Zb 36:5
Zb 103:11

b Zb 8:1
Zb 57:5, 11

c Zb 20:6
Zb 60:5

d Yos 17:7

e Mwa 33:17
Zb 60:6-8

f Yos 13:8, 11

g Kum 33:17

h Mwa 49:10

i 2Sa 8:2

j Hes 24:18
2Sa 8:14

k 2Sa 8:1

l Zb 60:9-12

Nami nitakuimbua sifa* miongoni mwa mataifa.

4 Kwa maana upendo wako mshikamanifu ni mku-bwa, uko juu kama mbingu,^a

Na uaminifu wako, unafika mpaka angani.

5 Ukwezwe juu ya mbingu, Ee Mungu; Utukufu wako na uwe juu ya dunia yote.^b

6 Ili wapendwa wako waokolewe, Tuokoe kwa mkono wako wa kuume na unijibu.^c

7 Mungu ameongea katika utakatifu wake:* "Nitashangilia, nitawagawia Shekemu^d kuwa urithi,

Nami nitawapimia Bonde la^e Sukothi.^e

8 Gileadi^f ni yangu, na Manase ni yangu, Na Efraimu ni kofia ya kuinga* kichwa changu;^g Yuda ni fimbo yangu ya kiongozi.^h

9 Moabu ni beseni langu la kuogea.ⁱ Nitatupa kiatu changu juu ya Edomu.^j

Nitapaza sauti kwa ushindi juu ya Ufilisti."^k

10 Ni nani atakayenipeleka kwenye lile jiji lenye ngome?

Ni nani atakayeniongoza mpaka Edomu?^l

11 Je, si wewe, Ee Mungu, ambaye umetukataa, Mungu wetu, ambaye

108:3 *Au "nitakupigia muziki." 108:7 *Au labda, "mahali pake patakatifu." #Au "Nchi Tambarare ya Chini ya." 108:8 *Tnn., "ngome ya."

haendi tena na majeshi yetu?^a

- 12 Tusaidie katika taabu yetu,^b

Kwa maana wokovu kuto-
ka kwa wanadamu hauna
faida yoyote.^c

- 13 Kwa msaada wa Mungu tu-
tapata nguvu,^d
Naye atawakanyagia chini
maadui wetu.^e

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

109 Ee Mungu ninayeku- sifu,^f usinyamaze.

- 2 Kwa maana waovu na
wadanganyifu hufumbua
vinywa vyao dhidi yangu.

Wanaongea kunihusu kwa
ndimi za uwongo;^g

- 3 Wanazingira kwa mane-
no ya chuki,
Na kunishambulia bila
sababu.^h

- 4 Wanapinga licha ya kwa-
mba ninawapenda;ⁱ

Lakini ninaendelea kusali.

- 5 Wanailipa uovu kwa
mema niliyotenda^j
Na chuki kwa upendo
wangu.^k

- 6 Mweke mtu mwovu amhu-
kumu;
Mpinzani* na asimame
mkono wake wa kulia.

- 7 Anapohukumiwa, na apa-
tikane kuwa na hatia;*
Hata sala yake ihesabiwe
kuwa dhambi.^l

- 8 Siku zake na ziwe
chache;^m

Mtu mwingine na achukue
cheo chake cha uangali-
lizi.ⁿ

- 9 Watoto wake* na wawe
mayatima,
Na mke wake awe mjane.

109:6 *Au "Mshtaki." 109:7 *Au "mwovu." 109:9 *Tnn., "Wanawe."

SURA YA 108

a Kum 23:14

b Zb 18:6

c Zb 118:8
Zb 146:3, 4

d 1Sa 2:4
2Sa 22:40
Isa 40:29-31

e Zb 44:5

SURA YA 109

f Zb 33:1

g 2Sa 15:2, 3
Zb 31:18

h 2Sa 15:12
2Sa 16:5-7
Zb 69:4

i 2Sa 13:39

j Zb 35:11, 12
Zb 38:19, 20

k Zb 55:12-14

l Isa 1:15
Mik 3:4

m Zb 55:23
Mt 27:5

n Mdo 1:16-20

Safu ya 2

a Zb 37:28

b 2Sa 3:28, 29
2Sa 21:1

c Zb 34:16

d Yak 2:13

e Zb 10:2

f 2Sa 16:11
2Sa 17:1, 2
Zb 37:32

- 10 Watoto wake* na watange-
tange wakiombaomba,
Wakitafuta chakula katika
nyumba zao zilizohari-
biwa.

- 11 Anayemdai na achukue
kwa nguvu* vitu vyote
alivyo navyo,
Wageni na wapore mali
zake.

- 12 Asiwepo mtu yeyote wa
kumtendea kwa fadhili,*
Na asiwepo mtu yeyote
wa kuwahurumia watoto
wake mayatima.

- 13 Wazao wake na waangami-
zwe;*^a
Jina lao na lifutwe katika
kizazi kilekile.

- 14 Kosa la mababu zake na li-
kumbukwe na Yehova,^b
Na dhambi ya mama yake
isifutwe.

- 15 Yehova na akumbuke dai-
ma waliyotenda;
Na afutilie mbali kumbu-
kumbu lao kutoka
duniani.^c

- 16 Kwa maana hakukumbuka
kutenda kwa fadhili,*^d
Bali aliendelea kumfuatia
mtu aliyekandamizwa,^e
maskini, na aliyevunjika
moyo

li amue.^f

- 17 Alipenda kulaani, kwa
hiyo laana hiyo ika-
mpata;
Hakupenda kubariki, kwa
hiyo hakupata baraka
yoyote.

- 18 Alivishwa laana kama vazi
lake.

109:10 *Au "Wanawe." 109:11 *Au "Wala riba na waviwekee mitego." 109:12, 16 *Au "upendo mshikamanifu." 109:13 *Au "Kizazi chake kijacho na kiangamizwe."

Nazo zikamwagwa mwilini mwake kama maji, Mifupani mwake kama mafuta.

- 19** Laana zake na ziwe kama vazi analojifunika^a
Na kama mshipi anaovaa daima.
- 20** Hayo ndiyo malipo yanayotoka kwa Yehova ya mtu anayenipinga^b
Na ya wale wanaosema mambo maovu dhidi yangu.
- 21** Lakini wewe, Yehova Bwana Mwenye Enzi Kuu, Tenda kwa niaba yangu kwa ajili ya jina lako.^c
Niokoe, kwa sababu upendo wako mshikamanifu ni mwema.^d
- 22** Kwa maana sina uwezo, nami ni maskini,^e
Na moyo wangu umechomwa ndani yangu.^f
- 23** Ninapitilia mbali kama kivuli kinachofifia; Nimekung'utwa kama nzige.
- 24** Magoti yangu yanalegea kwa sababu ya kufunga; Mwili wangu umekonda, unazidi kupungua.*
- 25** Nimekuwa kitu cha kudhihakiwa nao.^g
Wanaponiona, wanatikisa vichwa vyao.^h
- 26** Nisaidie, Ee Yehova Mungu wangu;
Niokoe kwa upendo wako mshikamanifu.
- 27** Na wajue kwamba mkono wako ndio uliotenda hili; Kwamba wewe, Ee Yehova, umetenda hili.
- 28** Waache watangaze laana, lakini wewe toa baraka.

109:24 *Tnn., "Mwili wangu umekuwa mwembamba, hauna mafuta."

SURA YA 109

a Zb 109:29

b 2Sa 17:23

c Zb 25:11
Zb 31:3d Zb 36:7
Zb 69:16
Zb 86:5

e Zb 40:17

f Zb 102:4

g Zb 31:11

h Zb 22:7
Mt 27:39

Safu ya 2

a Zb 35:26

b Zb 22:22

SURA YA 110

c Ro 8:34
Efe 1:20
Ebr 8:1
Ebr 12:2d Mt 22:43, 44
Mk 12:36
Lu 20:42, 43
Mdo 2:34, 35
1Ko 15:25
Ebr 1:3, 13
Ebr 10:12, 13e Zb 2:8, 9
Zb 45:4, 5
Mt 28:18
Ufu 6:2
Ufu 12:5
Ufu 19:11, 15

f Ebr 7:21, 28

g Mwa 14:18
Ebr 5:5, 6
Ebr 6:19, 20
Ebr 7:3, 11

Na waaibishwe wanapoinuka dhidi yangu, Lakini acha mtumishi wako ahangilie.

- 29** Wale wanaonipinga na wavisshwe aibu;
Na wafunikwe na aibu yao kama joho.*^a
- 30** Kinywa changu kitamsifu Yehova kwa bidii;
Nitamsifu yeye mbele ya watu wengi.^b
- 31** Kwa maana atasimama mkono wa kulia wa maskini
Ili amwokoe kutoka kwa wale wanaomhukumu.

Muziki wa Daudi.

110

Yehova alimtangazia hivi Bwana wangu:

"Keti kwenye mkono wangu wa kuume^c

Mpaka nitakapowaweka maadui wako kuwa kiti cha miguu yako."^d

- 2** Yehova atainyoosha fimbo ya ufalme ya nguvu zako kutoka Sayuni, akisema: "Nenda ukitiisha kati ya maadui wako."^e
- 3** Watu wako watajitoa kwa hiari katika siku ya jeshi lako.*

Katika utakatifu wenye fahari, kutoka katika tumbo la uzazi la mapambazuko,

Una kundi lako la vijana kama matone ya umande.

- 4** Yehova ameapa naye hatabadili nia yake:*
"Wewe ni kuhani milele^f
Kwa mfano wa Melkizedeki!"^g

109:29 *Au "joho lisilo na mikono."
110:3 *Au "siku ambayo jeshi lako litakusanyika." 110:4 *Au "hataghairi."

5 Yehova atakuwa kwenye mkono wako wa kulia;^a Atawaponda wafalme katika siku ya hasira yake.^b

6 Atatekeleza hukumu dhidi ya* mataifa;^c Atajaza maiti nchini.^d Atamponda kiongozi wa* nchi kubwa sana.^Δ

7 Atakunywa* maji ya kijito kilicho kando ya barabara. Kwa hiyo, atakiinua juu ki-chwa chake.

111 Msifuni Yah!*

Ⲛ [Aleph]
Nitamsifu Yehova kwa moyo wangu wote^f

ⲓ [Beth]
Katika kikundi kilichokusanyika cha watu wanyoofu na katika kutaniko.

ⲓ [Gimef]
2 Kazi za Yehova ni kuu;^g ⲓ [Daleth]

Wale wote wanaopendekwa nazo hujifunza kuzihusu.^h

ⲓ [He]
3 Utendaji wake ni wenye utukufu na fahari,

ⲓ [Waw]
Na uadilifu wake unadumu milele.ⁱ

ⲓ [Zayin]
4 Hufanya kazi zake zinazostaajibisha zikumbukwe.^j

ⲓ [Heth]
Yehova ni mwenye

110:6 *Au "miongoni mwa." #Tnn., "Ataponda kichwa cha." ΔAu "dunia nzima." 110:7 *Anayerejelewa ni "Bwana wangu" anayetajwa katika mstari wa 1. 111:1 *Au "Haleluya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova.

SURA YA 110

a Zb 16:8

b Zb 2:2
Ro 2:5
Ufu 11:18
Ufu 19:19

c Zb 79:6

d Yer 25:31-33

SURA YA 111

e Zb 68:4
Zb 113:1
Ufu 19:1

f Zb 9:1

g Zb 98:1
Zb 139:14
Ufu 15:3

h Zb 77:12
Zb 143:5

i Zb 103:17

j Kum 31:19
Yos 4:5-7

Safu ya 2

a Kut 34:6
Yak 5:11

b Zb 37:25
Mt 6:33

c Zb 89:34
Zb 105:8

d Zb 44:2
Zb 105:44

e Kum 32:4

f Zb 19:8
Isa 55:10, 11

g Zb 19:9

h Kut 15:13
Lu 1:68
Ufu 7:10

i Zb 89:7
Isa 6:2, 3
Lu 1:49
Ufu 4:8

j Ayu 28:28
Met 1:7
Mhu 12:13

k Kum 4:6
Yos 1:7, 8
1Fa 2:3
Zb 119:100
2Ti 3:14, 15

huruma* na mwenye rehema.^a

ⲓ [Teth]

5 Huwapa chakula wale wanaomwogopa.^b

ⲓ [Yod]

Hukumbuka agano lake milele.^c

ⲓ [Kaph]

6 Amewafunulia watu wake kazi zake zenye nguvu

ⲓ [Lamed]

Kwa kuwapa urithi wa mataifa.^d

ⲓ [Mem]

7 Kazi za mikono yake ni kweli na haki;^e

ⲓ [Nun]

Maagizo yake yote yanategemeka.^f

ⲓ [Samekh]

8 Yanategemeka* sikuzote, sasa na milele;

ⲓ [Ayin]

Msingi wake ni kweli na uadilifu.^g

ⲓ [Pe]

9 Amewakomboa watu wake.^h

ⲓ [Tsade]

Aliamuru kwamba agano lake linapaswa kudumu milele.

ⲓ [Qoph]

Jina lake ni takatifu na linaogopesha.ⁱ

ⲓ [Resh]

10 Kumwogopa Yehova ni mwanzo wa hekima.^j

ⲓ [Sin]

Wale wote wanaotii maagizo yake wana ufahamu mzuri.^k

ⲓ [Taw]

Sifa yake hudumu milele.

111:4 *Au "neema." 111:8 *Au "Yana msingi mzuri."

112 Msifuni Yah! *^a

N [Aleph]

Mwenye furaha ni mtu
anayemwogopa Yehova,^b

Q [Beth]

Anayependezwa sana na
amri zake.^c

J [Gimel]

2 Wazao wake watakuwa-
nye nguvu duniani,

T [Daleth]

Na kizazi cha mtu mnyoo-
fu kitabarikiwa.^d

K [He]

3 Nyumbani mwake mna
mali na utajiri,

L [Waw]

Na uadilifu wake unadumu
milele.

M [Zayin]

4 Yeye humwanzia
mnyoofu kama nuru
gizani.^e

N [Heth]

Ni mwenye huruma* na
mwenye rehema^f na ni
mwadilifu.

O [Teth]

5 Mambo humwendea vema
mtu anayekopesha kwa
ukarimu.*^g

P [Yod]

Hufanya mambo yake kwa
haki.

Q [Kaph]

6 Hatatikiswa kamwe.^h

R [Lamed]

Mwadilifu atakumbukwa
milele.ⁱ

S [Mem]

7 Hataogopa habari mbaya.^j

T [Nun]

Moyo wake ni imara, una-
mtumaini Yehova.^k

SURA YA 112

a Kut 15:2
Ufu 19:1

b Zb 111:10

c Zb 1:1, 2
Zb 40:8

d Zb 25:12, 13
Zb 37:25, 26

e Zb 97:11
1Pe 2:9

f Lu 6:36
Efe 4:32

g Kum 15:7, 8
Zb 41:1
Met 19:17
Lu 6:34, 35
Mdo 20:35
Ebr 13:16

h Zb 15:5
Zb 125:1

i Ne 5:19
Met 10:7

j Zb 27:1
Met 3:25

k Zb 62:8
Isa 26:3

Safu ya 2

a Met 28:1

b Zb 59:10

c Kum 15:11
Met 11:24
Met 19:17

d Kum 24:12, 13
2Ko 9:9
Ebr 6:10

e Met 11:7

SURA YA 113

f 1Nya 16:36
1Nya 29:10
Zb 106:48

g Zb 72:19
Zb 86:9
Isa 59:19
Mal 1:11

h Zb 97:9
Zb 99:2

i 1Fa 8:27

j Kut 15:11

Q [Samekh]

8 Moyo wake hauwezi kuti-
kiswa,* haogopi;^a

R [Ayin]

Hatimaye atawatazama
maadui wake wakishi-
ndwa.^b

S [Pe]

9 Amegawa kwa wingi,*
amewapa maskini.^c

T [Tsade]

Uadilifu wake unadumu
milele.^d

U [Qoph]

Nguvu zake mwenyewe
zitakwezwa* kwa utu-
kufu.

V [Resh]

10 Mwovu ataona na kukasi-
rika.

W [Shin]

Atasaga meno yake na ku-
yeyuka.

X [Taw]

Tamaa za mwovu zita-
ngamia.^e

113 Msifuni Yah!*

Msifuni, enyi watu-
mishi wa Yehova,

Lisifuni jina la Yehova.

2 Jina la Yehova na lisifiwe
Kuanzia sasa mpaka
milele.^f

3 Kuanzia jua linapochomo-
za mpaka linapotua,
Jina la Yehova na lisifiwe.^g

4 Yehova yuko juu zaidi ya
mataifa yote;^h
Utukufu wake uko juu ya
mbingu.ⁱ

5 Ni nani aliye kama Yehova
Mungu wetu,^j
Anayekaa juu?*

112:8 *Au "ni thabiti; ni imara." **112:9** *Au "kwa ukarimu." ^aTnn., "Pembe yake mwenyewe itakwezwa." **113:5** *Au "Anayeketi juu kwenye kiti cha ufalme?"

112:1; 113:1 *Au "Haleluya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova. **112:4** *Au "neema." **112:5** *Au "fadhili."

- 6 Huinama chini ili atazame mbingu na dunia,^a
- 7 Akimwinua mtu wa hali ya chini kutoka mavumbini. Humwinua juu maskini kutoka kwenye rundo la majivu.*^b
- 8 Ili amketishe pamoja na viongozi, Pamoja na viongozi wa watu wake.
- 9 Humpa makao mwanamke tasa Kama mama mwenye furaha aliye na watoto.*^c Msifuni Yah![#]

114 Israeli alipotoka Misri,^d

- Nyumba ya Yakobo ilipotoka kati ya watu waliozungumza lugha ya kigeni,
- 2 Yuda ikawa mahali pake patakatifu, Israeli, miliki yake.^e
- 3 Bahari iliona hilo na kukiambia;^f Mto Yordani ukarudi nyuma.^g
- 4 Milima ilirukaruka kama kondoo dume,^h Vilima, kama wanakondoo.
- 5 Ee bahari, ni nini kilichofanya ukimbie?ⁱ Ee Yordani, kwa nini ulirudi nyuma?^j
- 6 Enyi milima, kwa nini mlirukaruka kama kondoo dume, Kama wanakondoo, enyi vilima?
- 7 Tetemeka, Ee dunia, kwa sababu ya Bwana,

113:7 *Au labda, "jaa la takataka."
113:9 *Tnn., "wana." #Au "Haleluya!"
"Yah" ni ufupisho wa jina Yehova.

SURA YA 113

a Zb 18:35
Zb 138:6
Isa 57:15
Isa 66:2

b 1Sa 2:7

c 1Sa 2:5
Isa 54:1

SURA YA 114

d Kut 12:41

e Kut 6:7
Kut 19:6
Kum 32:9

f Kut 14:21

g Yos 3:16

h Kut 19:18
Amu 5:4

i Kut 15:8

j Yos 4:23

Safu ya 2

a 1Nya 16:29, 30

b Kut 17:6
Hes 20:11
Kum 8:14, 15
Zb 107:35

SURA YA 115

c Isa 48:11
Yoh 12:28

d Zb 138:2

e Kut 32:12
Hes 14:15, 16
Kum 32:26, 27
Zb 79:10

f Zb 135:15-18
Isa 40:19
Isa 46:6
Yer 10:3, 4
Yer 10:8, 9
Mdo 19:26
1Ko 10:19

g Hab 2:19

h 1Sa 5:3
Isa 46:7

i Hab 2:18

j Isa 44:9

k Zb 97:7

l Met 3:5

Kwa sababu ya Mungu wa Yakobo,^a

- 8 Anayeubadili mwamba kuwa dimbwi la maji lenye matete, Mwamba mgumu kuwa chemchemi za maji.^b

115 Usitutukuze sisi, Ee Yehova, usitutukuze sisi,*

Bali litukuze jina lako^c

Kwa sababu ya upendo wako mshikamanifu na uaminifu wako.^d

- 2 Kwa nini mataifa yaseme: "Yuko wapi Mungu wao?"^e
- 3 Mungu wetu yuko mbinguni; Hufanya lolote apendalo.
- 4 Sanamu zao ni fedha na dhahabu, Kazi ya mikono ya mwana-damu.^f
- 5 Zina kinywa, lakini haziwezi kuongea;^g Zina macho, lakini haziwezi kuona;
- 6 Zina masikio, lakini haziwezi kusikia;
- Zina pua, lakini haziwezi kunusa;
- 7 Zina mikono, lakini haziwezi kugusa;
- Zina miguu, lakini haziwezi kutembea;^h Hazitoi sauti yoyote kwa koo zake.ⁱ
- 8 Watu wanaozitengeneza watakuwa kama sanamu hizo,^j Na pia wote wanaozitumaini.^k
- 9 Ee Israeli, mtumainini Yehova!^l

115:1 *Au "Hatustahili chochote, Ee Yehova, hatustahili chochote."

—Yeye ndiye msaada wenu na ngao yenu.^a

10 Ee nyumba ya Haruni,^b mtumainini Yehova;

—Yeye ndiye msaada wenu na ngao yenu.

11 Ninyi mnaomwogopa Yehova, mtumainini Yehova^c

—Yeye ndiye msaada wenu na ngao yenu.^d

12 Yehova anatukumbuka na atatubariki;

Ataibariki nyumba ya Israeli;^e

Ataibariki nyumba ya Haruni.

13 Atawabariki wale wanaomwogopa Yehova, Wadogo kwa wakubwa.

14 Yehova atawapa ongezeko,

Ninyi na watoto* wenu.^f

15 Yehova na awabariki,^g Muumba wa mbingu na dunia.^h

16 Mbingu ni za Yehova,ⁱ Lakini dunia amewapa wanadamu.^j

17 Watu waliokufa hawamsifu Yah;^k

Wala yeyote anayeshuka kwenye ukimya wa kifo.^{*l}

18 Lakini sisi tutamsifu Yah Kuanzia sasa mpaka milele.

Msifuni Yah!^{*}

116 Ninampenda Yehova Kwa sababu yeye huisikia* sauti yangu, sihi zangu za kuomba msaada.^m

115:14 *Tnn., “wana.” **115:17** *Tnn., “kwenye kimya.” **115:18** *Au “Halelu-ya!” “Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. **116:1** *Au labda, “Ninapenda kwa sababu Yehova huisikia.”

SURA YA 115

a Kum 33:29
Zb 33:20

b Kut 28:1

c Met 16:20

d Zb 84:11

e Mwa 12:2

f Mwa 13:16

g Zb 3:8

h Zb 96:5

i Isa 66:1

j Mwa 1:28
Zb 37:29
Isa 45:18
Mdo 17:26

k Zb 6:5
Mhu 9:5

l Zb 31:17

SURA YA 116

m Zb 18:6

Safu ya 2

a Zb 34:15

b Isa 38:10

c Zb 18:4
Zb 38:6

d Zb 34:6
Ro 10:13

e Kum 32:4

f Kut 34:6
Ne 9:17
Da 9:9

g Zb 19:7

h Zb 56:13
Zb 94:18

i 2Ko 4:13

j Ro 3:4

2 Kwa maana yeye hunitegea sikio lake.^{*a}

Nami nitamlilia maadamu ninaishi.[#]

3 Kamba za kifo zilinizunguka;

Kaburi lilinishika kwa nguvu.^{*b}

Nililemewa na taabu na huzuni.^c

4 Lakini nikaliita jina la Yehova:^d

“Ee, Yehova, niokoe!”^{*}

5 Yehova ni mwenye huruma* na ni mwadilifu;^e

Mungu wetu ni mwenye rehema.^f

6 Yehova anawalinda wasio na uzoefu.^g

Nilishushwa chini, akanio-koa.

7 Acha nafsi* yangu ipumzi-ke tena,

Kwa maana Yehova ameni-tendea kwa fadhili.

8 Umeniokoa* kutoka kati-ka kifo,

Jicho langu kutokana na machozi, mguu wangu usijikwae.^h

9 Nitatembea mbele za Yehova katika nchi ya walio hai.

10 Nilikuwa na imani, ndio maana niliongea;ⁱ Niliteseka sana.

11 Basi nikashikwa na hofu na kusema:

“Kila mwanadamu ni mwongo.”^j

116:2 *Au “huinama chini ili kunisikiliza.” #Tnn., “katika siku zangu.” **116:3** *Tnn., “Nilipatwa na taabu za Sheoli.”

116:4 *Au “iokoe nafsi yangu.” **116:5** *Au “neema.” **116:7** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **116:8** *Au “Umeiokoa nafsi yangu.”

- 12** Nitamlipa Yehova nini
Kwa mema yote aliyonite-
ndea?
- 13** Nitakiinua kikombe cha
wokovu,*
Nami nitaliitia jina la
Yehova.
- 14** Nitamtimizia Yehova
nadhiri zangu
Mbele ya watu wake
wote.^a
- 15** Ni chenye thamani sana*
machoni pa Yehova
Kifo cha washikamanifu
wake.^b
- 16** Ninakusihi, Ee Yehova,
Kwa maana mimi ni mtu-
mishi wako.
Mimi ni mtumishi wako,
mwana wa kijakazi wako.
Umezifungua pingu
zangu.^c
- 17** Nitakutolea dhahibu ya
shukrani,^d
Nitaliitia jina la Yehova.
- 18** Nitamtimizia Yehova
nadhiri zangu^e
Mbele ya watu wake wote,^f
- 19** Katika nyua za nyumba ya
Yehova,^g
Kati yako, Ee Yerusalemu.
Msifuni Yah!^{*h}

- 117** Msifuni Yehova, enyi
mataifa yote;ⁱ
Mtukuzeni, enyi mataifa
yote.^{*j}
- 2** Kwa maana upendo wake
mshikamanifu kutuele-
kea ni mkubwa;^k
Uaminifu/ wa Yehova una-
dumu milele.^m
Msifuni Yah!^{*n}

116:13 *Au "wokovu mkuu." **116:15**
*Au "Ni cha bei kubwa sana." **116:19;**
117:2 *Au "Haleluya!" "Yah" ni ufupisho
wa jina Yehova. **117:1** *Au "koo zote."

SURA YA 116

a Zb 22:25
Yon 2:9

b 1Sa 25:29
Ayu 1:12
Zb 91:14
Zek 2:8
2Pe 2:9

c Zb 107:14

d Law 7:12
Zb 50:23

e Zb 22:25
Zb 76:11

f Zb 116:14

g Zb 96:8

h Ufu 19:1

SURA YA 117

i Ufu 7:9, 10

j Ro 15:11

k Omb 3:22

l Zb 25:10
Zb 91:4

m Zb 100:5

n Zb 111:1

Safu ya 2

SURA YA 118

a Mt 19:17

b Zb 18:19

c Zb 27:1

d Isa 51:12
Ro 8:31
Ebr 13:6

e Mt 26:52, 53

f Zb 54:7

g Zb 40:4
Zb 146:3, 4
Yer 17:5

h Eze 29:6, 7

i 2Nya 20:15, 17

118 Mshukuruni Yehova,
kwa maana yeye ni
mwema;^a

- Upendo wake mshikamani-
fu unadumu milele.
- 2** Watu wa Israeli na wase-
me sasa:
"Upendo wake mshikama-
nifu unadumu milele."
- 3** Watu wa nyumba ya Haru-
ni na waseme sasa:
"Upendo wake mshikama-
nifu unadumu milele."
- 4** Wale wanaomwogopa Ye-
hova na waseme sasa:
"Upendo wake mshikama-
nifu unadumu milele."
- 5** Nilimlilia Yah* nilipokuwa
nikitaabika;
Yah akanijibu na kunipele-
ka mahali salama.^{#b}
- 6** Yehova yuko upande
wangu; sitaogopa.^c
Mwanadamu atanifanya
nini?^d
- 7** Yehova yuko upande
wangu akiwa msaidizi
wangu;^{*e}
Wale wanaonichukia nita-
watazama wakishindwa.^f
- 8** Ni bora kumkimbilia Ye-
hova
Kuliko kuwatumaini wana-
damu.^g
- 9** Ni bora kumkimbilia
Yehova
Kuliko kuwatumaini
wakuu.^h
- 10** Mataifa yote yalinizingira,
Lakini katika jina la
Yehova,
Niliyafukuza.ⁱ
- 11** Yalinizingira, naam, yali-
nizingira kabisa,

118:5 *"Yah" ni ufupisho wa jina Yeho-
va. #Au "mahali penye nafasi kubwa."
118:7 *Au labda, "pamoja na wale wa-
naonisaidda."

- Lakini katika jina la Yehova, Niliyafukuza.
- 12** Yalinizingira kama nyuki, Lakini yalizimwa haraka kama moto unaoteketeza miiba.
Katika jina la Yehova, Niliyafukuza.^a
- 13** Nilisukumwa kwa nguvu* ili nianguke, Lakini Yehova alinisaidia.
- 14** Yah ni mahali pangu pa kujificha na nguvu zangu, Naye amekuwa wokovu wangu.^b
- 15** Sauti ya shangwe na wokovu* Imo katika mahema ya waadilifu. Mkono wa kuume wa Yehova unaonyesha nguvu zake.^c
- 16** Mkono wa kuume wa Yehova unajikweza; Mkono wa kuume wa Yehova unaonyesha nguvu zake.^d
- 17** Sitakufa, hapana, nitaishi, Ili nizitangaze kazi za Yah.^e
- 18** Yah aliniadhibu vikali,^f Lakini hakunitia mikononi mwa kifo.^g
- 19** Nifungulieni malango ya uadilifu;^h Nitaingia humo na kumsifu Yah.
- 20** Hili ndilo lango la Yehova. Waadilifu wataingia humo.ⁱ
- 21** Nitakusifu, kwa maana ulinijibu^j

118:13 *Au labda, "Ulinisukuma kwa nguvu." **118:15** *Au "ushindi."

SURA YA 118

a 2Nya 14:11

b Kut 15:2
Zb 18:2
Isa 12:2c Zb 89:13
Isa 63:12d Kut 15:6
Isa 40:26e Zb 6:5
Zb 71:17f Zb 66:10
Zb 94:12

g Zb 16:10

h Isa 26:2
Ufu 22:14

i Zb 24:3, 4

j Zb 116:1

Safu ya 2

a Isa 28:16
Lu 20:17
Mdo 4:11
1Ko 3:11
Efe 2:19, 20
1Pe 2:4-7

b Mdo 5:31

c Mk 12:10, 11

d Mt 21:7-9
Mt 23:39
Mk 11:7-10
Lu 19:37, 38e Zb 18:28
1Pe 2:9f Law 23:34
Zb 42:4

g Kut 27:2

h Kut 15:2
Isa 25:1

i Zb 50:23

j Ezr 3:11
Zb 118:1

Nawe ukawa wokovu wangu.

- 22** Jiwe ambalo wajenzi walilikataa Limekuwa jiwe kuu la pembeni.^{*a}
- 23** Hili limetoka kwa Yehova;^b Linastaajabisha machoni petu.^c
- 24** Hii ndiyo siku ambayo Yehova ameifanya; Tutaishangilia na kuifuraha.
- 25** Yehova, tuokoe, tafadhali, tunakusihii! Yehova, tupe ushindi, tafadhali!
- 26** Amebarikiwa yule anayekuja katika jina la Yehova;^d Tunakubariki kutoka katika nyumba ya Yehova.
- 27** Yehova ni Mungu; Hutupatia nuru.^e Mkiwa na matawi mikononi jiungeni na maandamano ya sherehe,^f Mpaka kwenye pembe za madhabahu.^g
- 28** Wewe ni Mungu wangu, nami nitakusifu; Mungu wangu, nitakuweza.^h
- 29** Mshukuruni Yehova,ⁱ kwa maana yeye ni mwema; Upendo wake mshikamanifu unadumu milele.^j
- ⲛ [Aleph]
- 119** Wenye furaha ni wale wasio na lawama* katika njia yao,

118:22 *Tnn., "kichwa cha pembeni."
119:1 *Au "wanaoshika utimilifu."

- Wanaotembea katika sheria ya Yehova.^a
- 2** Wenye furaha ni wale wanaoshika vikumbusho vyake,^b
Wanaomtafuta kwa moyo wao wote.^c
- 3** Hawatendi uovu wowote; Wanatembea katika njia zake.^d
- 4** Umeamuru Kwamba maagizo yako yafuatwe kwa uangalifu.^e
- 5** Laiti ningeweza kubaki imara*^f
Ili niyashike masharti yako!
- 6** Ndipo sitaambishwa^g
Ninapokazia uangalifu amri zako zote.
- 7** Nitakusifu kwa moyo mnyoofu
Ninapojifunza hukumu zako za uadilifu.
- 8** Nitayashika masharti yako. Kamwe usiniache kabisa.
☩ [Beth]
- 9** Kijana anaweza kuisafishaje njia yake?
Kwa kujilinda kulingana na neno lako.^h
- 10** Ninakutafuta kwa moyo wangu wote.
Usiache nikengeuke kutoka katika amri zako.ⁱ
- 11** Ninaweka neno lako moyoni mwangu kama hazina^j
Ili nisikutendee dhambi.^k
- 12** Na usifiwe, Ee Yehova; Nifundishe masharti yako.

119:5 *Tnn., "Laiti njia zangu zingekuwa zimeimarishwa kabisa."

SURA YA 119

a 2Fa 20:3
Yak 1:25

b Zb 19:7

c 2Nya 31:20, 21

d Isa 38:3

e Kum 5:33
Yer 7:23
Yak 2:10

f Zb 51:10

g Zb 119:80

h Met 6:20, 22

i Zb 25:5

j Zb 112:1

k Zb 19:13
Zb 37:31

Safu ya 2

a Yer 15:16

b Zb 19:8, 10
Zb 119:72

c Zb 119:93
Zb 119:100

d Zb 25:10

e Yak 1:23-25

f Isa 38:20

g 1Nya 29:15

h Kum 28:15

13 Kwa midomo yangu nina-tangaza
Hukumu zote ulizonena.

14 Ninashangilia kwa sababu ya vikumbusho vyako^a
Kuliko vitu vingine vyote vyenye thamani.^b

15 Nitatafakari* maagizo yako^c
Na kuzikazia macho njia zako.^d

16 Ninazipenda sana sheria zako.
Sitalisahau neno lako.^e

λ [Gimef]

17 Nitendee kwa fadhili mimi mtumishi wako,
Ili niishi na kulishika neno lako.^f

18 Yafumbue macho yangu ili nione wazi
Mambo yanayostaajabisha katika sheria yako.

19 Mimi ni mgeni tu nchini.^g
Usinifiche amri zako.

20 Ninapondeka* kwa kutamani sana
Hukumu zako nyakati zote.

21 Unawakemea wenye ki-mbelembele,
Watu waliolaaniwa wanaokengeuka kutoka katika amri zako.^h

22 Niondolee* dhihaka na dharau,
Kwa maana nimeshika vikumbusho vyako.

23 Hata wakuu wanapoke-ti pamoja na kusema mambo mabaya kuni-husu,

119:15 *Au "Nitajifunza." 119:20 *Au "Nafsi yangu inapondeka." 119:22 *Tnn., "Vingirisha mbali nami."

Mimi mtumishi wako
ninatafakari* masharti
yako.

- 24 Ninavipenda sana viku-
mbusho vyako;^a
Navyo ni washauri
wangu.^b

† [Daleth]

- 25 Ninalala kifudufudi mavu-
mbini.^c
Nihifadhi hai kulingana
na neno lako.^d

- 26 Nilikwambia kuhusu njia
zangu, nawe ukanijibu;
Nifundishe masharti
yako.^e

- 27 Nifanye nielewe maana*
ya maagizo yako,
Ili niweze kutafakari#
kazi zako zinazostaaja-
bisha.^f

- 28 Nimekosa usingizi kwa
sababu ya huzuni.
Nitie nguvu kulingana na
neno lako.

- 29 Niondolee njia ya udanga-
nyifu,^g
Na unionyeshe kibali kwa
kunipa sheria yako.

- 30 Nimechagua njia ya uami-
nifu.^h
Ninatambua kwamba
hukumu zako zinafaa.

- 31 Ninashikamana na viku-
mbusho vyako.ⁱ
Ee Yehova, usiache nika-
tishwe tamaa.*^j

- 32 Nitaifuata kwa bidii* njia
ya amri zako
Kwa sababu wewe huufa-
nya moyo wangu uwe na
nafasi kwa ajili yake.*

119:23 *Au "ninajifunza." 119:27
*Tnn., "njia." #Au "kujifunza." 119:31
*Au "niaibishwe." 119:32 *Tnn., "Nita-
kimbia katika." #Au labda, "huufanya
moyo wangu uwe na ujasiri."

SURA YA 119

a Zb 119:14
Zb 119:168

b Kum 17:18-20
Zb 119:105
2Ti 3:16, 17

c Zb 22:15

d Zb 119:154
Zb 143:11

e Zb 86:11

f Zb 145:5

g Zb 141:4
Met 30:8

h Yos 24:15

i Zb 19:7

j Zb 25:20
Zb 119:80

Safu ya 2

a Isa 48:17
Yoh 6:45
Yak 1:5

b Zb 119:112

c Zb 23:3

d Lu 12:15
ITI 6:10
Ebr 13:5

e Hes 15:39
Met 4:25
Met 23:4, 5

f Zb 19:9
Zb 119:75

g Zb 51:1
Zb 90:14

h Zb 119:76

† [He]

- 33 Nifundishe, Ee Yehova,^a
njia ya masharti yako,
Nami nitaifuata mpaka
mwisho.^b

- 34 Nipe uelewaji,
Ili niweze kushika sheria
yako
Na kuitii kwa moyo wa-
ngu wote.

- 35 Niongoze* katika njia ya
amri zako,^c
Kwa maana ninapende-
zwa nayo.

- 36 Uelekeze moyo wangu
kwenye vikumbusho
vyako,
Wala si kwa tamaa ya* ki-
choyo.^d

- 37 Yageuzi mbali macho ya-
ngu yasitazame mambo
yasiyofaa;^e
Nihifadhi hai katika njia
yako.

- 38 Nitimizie mimi mtumishi
wako ahadi yako,*
Ili uogopwe.^f

- 39 Niondolee aibu ninayoo-
gopa sana,
Kwa maana hukumu zako
ni njema.^f

- 40 Tazama jinsi ninavyoya-
tamani sana maagizo
yako!
Nihifadhi hai katika uadi-
lifu wako.

† [Waw]

- 41 Acha nijionee upendo
wako mshikamanifu, Ee
Yehova,^g
Wokovu wako kulingana
na ahadi yako;*^h

- 42 Kisha nitamjibu yule ana-
yenidihiki,

119:35 *Au "Nitembeze." 119:36 *Au
"kwa faida za." 119:38, 41 *Au "neno
lako." 119:38 #Au labda, "Ambayo hu-
tolewa kwa wale wanaokuogopa."

- Kwa maana ninalitumaini neno lako.
- 43** Usiondoe kabisa neno la kweli kutoka kinywani mwangu,
Kwa maana nimetumaini* hukumu yako.
- 44** Nitaishika sheria yako daima,
Milele na milele.^a
- 45** Nami nitatembeatembea mahali salama,^{*b}
Kwa maana ninayatafuta maagizo yako.
- 46** Nitaongea kuhusu vikumbusho vyako mbele ya wafalme,
Nami sitaaibika.^c
- 47** Ninazipenda sana amri zako,
Naam, ninazipenda.^d
- 48** Nitainua mikono yangu kuelekea amri zako, ambazo ninazipenda,^e
Nami nitayatafakari* masharti yako.^f
† [Zayin]
- 49** Likumbuke neno lako ulilomwambia* mtumishi wako,
Ambalo kupitia hilo unanipa tumaini.[#]
- 50** Hilo ndilo faraja yangu katika mateso yangu,^g
Kwa maana neno lako limenihiifadhi hai.
- 51** Wenye kimbelebele wanandihahi sana,
Lakini sikengeuki kutoka kwenye sheria yako.^h

119:43 *Au "ninangojea." **119:45** *Au "mahali penye nafasi kubwa." **119:48** *Au "nitajifunza." **119:49** *Au "Kumbuka ahadi yako uliyompa." *Au "Ambalo ulinifanya nisubiri."

SURA YA 119

a Zb 119:33

b Zb 118:5

c Ro 1:16

d Ayu 23:12
Zb 119:174
Ro 7:22

e Zb 119:127

f Zb 119:23
Zb 119:71

g Zb 94:19
Ro 15:4

h Zb 119:157

Safu ya 2

a Hes 16:5
Kum 1:35, 36
Kum 4:3

b Ro 15:4

c Zb 119:158
Zb 139:21
Met 28:4

d Zb 63:6
Isa 26:9

e Zb 16:5

f Kut 19:8

g Zb 51:17

h Zb 57:1

i Zb 119:101
Efe 5:15

j 2Nya 29:1, 3

k 1Sa 26:8, 9
2Nya 29:1, 2

l Zb 42:8

- 52** Ninazikumbuka hukumu zako za tangu zamani,^a
Ee Yehova,
Nazo zinanifariji.^b
- 53** Nimeshikwa na hasira kali kwa sababu ya waovu,
Wanaoiacha sheria yako.^c
- 54** Masharti yako ni nyimbo kwangu
Popote ninapoishi.*
- 55** Wakati wa usiku ninalikumbuka jina lako, Ee Yehova,^d
Ili niweze kuishika sheria yako.
- 56** Nimezoea kufanya hivyo kwa sababu nimeyatii maagizo yako.
† [Heth]
- 57** Yehova ni fungu langu;^e
Nimeahidi kuyashika mawazo yako.^f
- 58** Ninakusihii* kwa moyo wangu wote;^g
Nionyeshe kibali^h kulingana na ahadi yako.[#]
- 59** Nimezichunguza njia zangu,
Ili niirudishe miguu yangu kwenye vikumbusho vyako.ⁱ
- 60** Ninafanya haraka wala sikawii
Kuzishika amri zako.^j
- 61** Kamba za waovu zinanzunguka,
Lakini siisahau sheria yako.^k
- 62** Katikati ya usiku ninaamka ili kukushukuru!^l

119:54 *Au "Katika nyumba ninamoishi kama mgeni." **119:58** *Au "Ninautuliza (ninatafuta tabasamu ya) uso wako." *Au "neno lako."

Kwa sababu ya hukumu
zako za uadilifu.

63 Mimi ni rafiki ya wote wa-
naokuogopa wewe

Na ya wale wanaoyatii
maagizo yako.^a

64 Upendo wako mshikama-
nifu, Ee Yehova, umeijaza
dunia;^b

Nifundishe masharti
yako.

☞ [Teth]

65 Umenitendea mema mimi
mtumishi wako,

Ee Yehova, kulingana na
neni lako.

66 Nifundishe busara na uju-
zi,^c

Kwa maana nimezitumai-
ni amri zako.

67 Kabla ya kuteswa, niliku-
wa nikikengeuka,^{*}

Lakini sasa ninalishika
neni lako.^d

68 Wewe ni mwema^e na kazi
zako ni njema.

Nifundishe masharti
yako.^f

69 Wenye kimbelebele hu-
nipaka uwongo,

Lakini ninayatii maagizo
yako kwa moyo wangu
wote.

70 Moyo wao umekufa ga-
nzi,^{*g}

Lakini ninaipenda sana
sheria yako.^h

71 Ni vema kwamba nimete-
swa,ⁱ

Ili nijifunze masharti
yako.

72 Sheria uliyotangaza ni
njema kwangu,^j

Kuliko maelfu ya vipande
vya dhahabu na fedha.^k

119:67 *Au "nilikuwa nikitenda dhambi bila kukusudia." **119:70** *Tnn., "hauna hisia, ni kama mafuta."

SURA YA 119

a Met 13:20

b Zb 33:5
Zb 104:13

c 1Fa 3:9
Zb 94:10
Da 2:21
Flp 1:9

d Zb 119:11

e Zb 86:5
Mk 10:18

f Isa 48:17

g Isa 6:10

h Zb 40:8
Ro 7:22

i 1Ko 11:32
Ebr 12:9-11

j Kum 17:18, 19

k Zb 19:7, 10
Met 3:13-15

Safu ya 2

a 1Nya 22:12
Ayu 32:8

b Zb 119:147

c Zb 119:160

d Kum 32:4
Ebr 12:11

e Kut 34:6
Zb 86:5

f Zb 51:1
Zb 103:13
Zb 119:116
Da 9:18
Lu 1:50

g Ro 7:22

h Zb 119:45

i 1Fa 8:58

j Zb 119:5, 6
1Yo 2:28

k Mik 7:7

[^] [Yod]

73 Mikono yako iliniumba na
kunifinyanga.

Nipe uelewaji,

Ili nijifunze amri zako.^a

74 Wale wanaokuogopa hu-
niona na kushangilia,

Kwa maana neni lako ni
tumaini langu.^{*b}

75 Ninajua, Ee Yehova, kwa-
mba hukumu zako ni za
uadilifu^c

Na kwamba umenitesa
kwa uaminifu wako.^d

76 Tafadhali, upendo wako
mshikamanifu^e na uni-
fariji,

Kulingana na ahadi yako
uliyonipa^{*} mimi mtumi-
shi wako.

77 Nionyeshe rehema ili nie-
ndelee kuishi,^f

Kwa maana ninaipenda
sana sheria yako.^g

78 Wenye kimbelebele na
waabishwe,

Kwa maana wananikosea
bila sababu.^{*}

Lakini nitayatafakari[#]
maagizo yako.^h

79 Acha wale wanaokuogopa
warudi kwangu,

Wale wanaojua vikumbu-
sho vyako.

80 Moyo wangu na uwe bila
lawama katika kufuata
masharti yako,ⁱ

Ili nisiaibishwe.^j

☞ [Kaph]

81 Ninautamani sana woko-
vu wako,^k

Kwa maana neni lako ni
tumaini langu.^{*}

119:74, 81 *Au "ninalingojea neni lako." **119:76** *Au "neni lako uliloni-pa." **119:78** *Au labda, "kwa kusema uwongo." [#]Au "nitajifunza."

- 82** Macho yangu yanatamani sana neno lako^a
Huku nikisema: “Utanifariji lini?”^b
- 83** Kwa maana mimi ni kama kiriba cha ngozi kilichokaushwa na moshi,
Lakini siyasahau masharti yako.^c
- 84** Mimi mtumishi wako nishubiri kwa siku ngapi?
Ni lini utakapowahukumu wale wanaonitesa?^d
- 85** Wenye kimbelebele wananichimbia mashimo,
Wale wanaoasi sheria yako.
- 86** Amri zako zote zinategemeka.
Watu wananitesa bila sababu; nisaidie!^e
- 87** Karibu waniangamize kutoka duniani,
Lakini sikuyaacha maagizo yako.
- 88** Nihifadhi hai kwa sababu ya upendo wako mshikamanifu,
Ili nishike vikumbusho ulivyosema.
↳ [Lamed]
- 89** Milele, Ee Yehova,
Neno lako litadumu mbinguni.^f
- 90** Uaminifu wako umekuwapo kwa vizazi vyote.^g
Umeimarisha kabisa dunia, ili idumu.^h
- 91** Kwa sababu ya hukumu zako zinadumu* mpaka leo,
Kwa maana zote ni watumishi wako.
- 92** Kama singeipenda sana sheria yako,

SURA YA 119

a Zb 69:3

b Zb 86:17
Zb 102:2c Zb 119:61
Zb 119:176d Zb 7:6
Ufu 6:9, 10

e Zb 142:6

f Zb 89:2
Zb 119:152

g Kum 7:9

h Zb 104:5
Mhu 1:4

Safu ya 2

a Met 6:23
Mt 4:4b Law 18:5
Kum 30:16
Yoh 6:63
Ro 10:5c Zb 86:2
Isa 41:10

d Zb 119:15

e Zb 40:8

f Zb 1:2

g Zb 19:7
Met 2:6
Met 10:8h Mt 11:25
Lu 2:46, 47i Zb 18:23
Zb 119:59Ningekuwa nimeangamia katika mateso yangu.^a**93** Sitayasahau kamwe maagizo yako,Kwa sababu kupitia hayo umenihifadhi hai.^b**94** Mimi ni wako; niokoe,^c
Kwa sababu nimeyatafuta maagizo yako.^d**95** Waovu wanasubiri kuniangamiza,

Lakini ninavikazia sana fikira vikumbusho vyako.

96 Nimeona mwisho wa ukamilifu wote,
Lakini amri yako haina mpaka.*

↳ [Mem]

97 Jinsi ninavyoipenda sana sheria yako!^e
Ninaitafakari* mchana kutwa.^f**98** Amri yako hunifanya niwe na hekima kuliko maadui wangu,^g

Kwa sababu ninayo milele.

99 Nina ufahamu mwingi kuliko walimu wangu wote,^h

Kwa sababu ninavitafakari* vikumbusho vyako.

100 Ninatenda kwa uelewaji mwingi kuliko wanaume wazee,

Kwa sababu ninayatii maagizo yako.

101 Ninakataa kutembea kwenye njia yoyote ya uovu,ⁱ
Ili nishike neno lako.**102** Sigeuki kando kutoka katika hukumu zako,
Kwa maana umenifundisha.**119:96** *Tnn., “ni pana sana.” **119:97** *Au “Ninajifunza kuihusu.” **119:99** *Au “ninajifunza.”**119:91** *Yaani, kazi zake zote za uumbaji.

- 103** Jinsi maneno yako ya-
livyo matamu kwenye
kaaka langu,
Kuliko asali kinywani
mwangu!^a
- 104** Kwa sababu ya maagizo
yako ninatenda kwa ue-
lewaji.^b
Ndiyo sababu ninaichu-
kia kila njia ya uwongo.^c
‡ [Num]
- 105** Neno lako ni taa ya mguu
wangu,
Na nuru ya njia yangu.^d
- 106** Nimeweka kiapo, nami ni-
takitimiza,
Kwamba nitazishika hu-
kumu zako za uadilifu.
- 107** Nimeteseka sana.^e
Ee Yehova, nihifadhi
hai kulingana na neno
lako.^f
- 108** Tafadhali yafurahie mato-
leo yangu ya hiari ya
kukusifu,^g Ee Yehova,
Na unifundishe hukumu
zako.^h
- 109** Uhai wangu umo hatarini
daima,^{*}
Lakini sijaisahau sheria
yako.ⁱ
- 110** Waovu wamenitegea mtego,
Lakini sijakengeuka ku-
toka katika maagizo
yako.^j
- 111** Ninavichukua vikumbu-
sho vyako kuwa mali
yangu ya kudumu,^{*}
Kwa maana hivyo ni sha-
ngwe ya moyo wangu.^k
- 112** Nimeazimia* kuyatii mah-
sharti yako

119:108 *Tnn., "matoleo ya hiari ya ki-
nywa changu." **119:109** *Au "Nafsi ya-
ngu imo mikononi mwangu daima."
119:111 *Au "urithi wangu wa milele."
119:112 *Tnn., "Nimeuelekeza moyo
wangu."

SURA YA 119

a Zb 19:7, 10
Met 24:13, 14

b Zb 119:100

c Zb 97:10
Zb 101:3
Met 8:13
Met 13:5
Ro 12:9

d Zb 43:3
Met 6:23
Isa 51:4
Ro 15:4
2Ti 3:16, 17
2Pe 1:19

e Zb 34:19

f Zb 119:88
Zb 143:11

g Zb 50:23
Ho 14:2
Ebr 13:15

h Kum 33:10
Isa 48:17

i Zb 119:61

j Zb 119:87

k Zb 19:8
Zb 119:129
Yer 15:16

Safu ya 2

a 1Fa 18:21
Ufu 3:16

b Zb 40:8
Zb 119:97

c Zb 32:7
Zb 91:2

d Zb 130:5

e Zb 26:5

f Isa 41:10

g Zb 25:2
Ro 10:11

h Isa 41:13

i Yos 1:8
Zb 119:48

j 1Nya 28:9
Zb 95:10

k Met 2:22
Met 25:4, 5
Eze 22:18

Nyakati zote, mpaka
mwisho.

‡ [Samekh]

- 113** Ninawachukia watu we-
nye moyo nusunusu,^{*a}
Lakini ninaipenda sheria
yako.^b
- 114** Wewe ni mahali pangu
pa kujificha na ngao
yangu,^c
Kwa maana neno lako ni
tumaini langu.^{*d}
- 115** Kaeni mbali nami, enyi
waovu,^e
Ili nizishike amri za
Mungu wangu.
- 116** Nitegemeze kama ulivyo-
ahidi,^{*f}
Ili niendelee kuishi;
Usiache tumaini langu li-
badilike na kunikatisha
tamaa.^{*g}
- 117** Nitegemeze ili nioko-
lewe,^h
Kisha nitayakazia unga-
lifu daima masharti
yako.ⁱ
- 118** Unawakataa wote wanao-
kengeuka kutoka katika
masharti yako,^j
Kwa maana ni waongo na
wadanganyifu.
- 119** Unawatupilia mbali wao-
vu wote walio duniani
kana kwamba ni taka-
taka.^{*k}
Ndiyo sababu ninavipe-
nda vikumbusho vyako.
- 120** Mwili wangu unatete-
meka kwa sababu ya
kukuhofu;
- 119:113** *Au "moyo uliogawanyika."
119:114 *Au "Ninalingojea neno
lako." **119:116** *Au "kulingana na
neno lako." *Au "liaibishwe." **119:119**
*Neno la Kiebrania linalotafsiriwa "taka-
taka" katika mstari huu linarejelea ucha-
fu unaotoka katika fedha au dhahabu
inapoyeyushwa.

Ninaogopa hukumu
zako.

‡ [Ayin]

121 Nimetenda yaliyo ya haki
na uadilifu.

Usiniache mikononi
mwa wale wanaonika-
ndamiza!

122 Nihakikishie hali njema
mimi mtumishi wako;
Wenye kimbelebele wa-
sinikandamize.

123 Macho yangu yamecho-
ka nikiungojea wokovu
wako^a

Na ahadi yako ya* uadi-
lifu.^b

124 Nitendee mimi mtumishi
wako kwa upendo mshi-
kamanifu,^c

Na unifundishe masharti
yako.^d

125 Mimi ni mtumishi wako;
nipe uelewaji,^e
Ili nijue vikumbusho
vyako.

126 Wakati umefika wa Yeho-
va kutenda,^f
Kwa maana wameivunja
sheria yako.

127 Ndiyo sababu ninazipe-
nda amri zako
Kuliko dhahabu, hata
dhahabu bora.*^g

128 Kwa hiyo, ninayaona
mafundisho* yote yana-
yotoka kwako kuwa
yanafaa;^h
Ninaichukia kila njia ya
uwongo.ⁱ

‡ [Pe]

129 Vikumbusho vyako ni vi-
zuri sana.
Ndiyo sababu ninavi-
shika.

119:123 *Au "neni lako la." 119:127
*Au "iliyosafishwa." 119:128 *Au
"maagizo."

SURA YA 119

a Zb 69:3
Zb 143:7

b Zb 119:81

c Zb 69:16

d Zb 143:10

e Zb 119:34
2Ti 2:7
Yak 1:5

f Zb 9:19
Yer 18:23

g Zb 19:9, 10
Zb 119:72
Met 3:13, 14

h Zb 19:8

i Zb 119:104

Safu ya 2

a Zb 119:105
Met 6:23
2Ko 4:6
2Pe 1:19

b Zb 19:7
Met 1:1, 4
2Ti 3:15

c Zb 42:1
1Pe 2:2

d 1Sa 1:10, 11
2Sa 16:11, 12
Isa 38:9, 20

e Ebr 6:10

f Zb 19:13
Ro 6:12

g Hes 6:25
Zb 4:6

h Eze 9:4
2Pe 2:7, 8

i Kum 32:4

j Ufu 16:5, 7

130 Kufunuliwa kwa maneno
yako huleta nuru,^a

Na humpa uelewaji mtu
asiye na uzoefu.^b

131 Ninakifumbua wazi ki-
nywa changu na kutweta,*
Kwa sababu ninazitamani
sana amri zako.^c

132 Nigeukie na kunionyesha
kibali,^d
Kama unavyowatendea*
wale wanaolipenda jina
lako.^e

133 Ziongoze hatua zangu
kwa usalama* kupitia
neni lako;
Jambo lolote ovu lisinita-
wale.^f

134 Niokoe* kutoka kwa
wanadamu wanaoka-
ndamiza,
Nami nitayatii maagizo
yako.

135 Ufanye uso wako unia-
ngazie* mimi mtumishi
wako,^g
Na unifundishe masharti
yako.

136 Macho yangu yanatiriri-
kwa na machozi
Kwa sababu watu hawatii
sheria yako.^h
‡ [Tsade]

137 Wewe ni mwadilifu, Ee
Yehova,ⁱ
Na hukumu zako ni za
haki.^j

138 Vikumbusho unavyotoa
ni vya uadilifu
Navyo vinategemeka
kabisa.

119:131 *Tnn., "kuhemahema."
119:132 *Tnn., "Kulingana na uamuzi
wako kuwaelekea." 119:133 *Au "Zifa-
nye hatua zangu ziwe imara." 119:134
*Tnn., "Nikomboe." 119:135 *Au "uta-
basamu kunielekea."

- 139** Bidii yangu inanila,^a
Kwa sababu maadui
wangu wameyasahau
maneno yako.
- 140** Neno lako ni safi kabisa,^b
Nami mtumishi wako ni-
nalipenda.^c
- 141** Mimi ni duni na mwenye
kudharauliwa;^d
Hata hivyo, sijayasahau
maagizo yako.
- 142** Uadilifu wako ni uadilifu
wa milele,^e
Na sheria yako ni kweli.^f
- 143** Hata nikipatwa na taabu
na shida,
Nitaendelea kuzipenda
sana amri zako.
- 144** Uadilifu wa vikumbusho
vyako ni wa milele.
Nipe uelewaji,^g ili niende-
lee kuishi.
𐤒 [Qoph]
- 145** Ninakuita kwa moyo wa-
ngu wote. Nijibu, Ee
Yehova.
Nitayashika masharti
yako.
- 146** Ninakulilia wewe; niokoe!
Nitashika vikumbusho
vyako.
- 147** Nimeamka kabla ya ma-
pambazuko* ili nililie
msaada,^h
Kwa maana maneno yako
ni tumaini langu.[#]
- 148** Macho yangu hufunguka
kabla ya makesha ya
usiku,
Ili nitafakari* neno lako.ⁱ
- 149** Isikie sauti yangu kwa sa-
babu ya upendo wako
mshikamanifu.^j
Ee Yehova, nihifadhi hai
kulingana na haki yako.

119:147 *Au "alfajiri." #Au "Ninayan-
ngojea maneno yako." 119:148 *Au
"nijifunze."

SURA YA 119

a 2Fa 10:16
Zb 69:9
Yoh 2:17

b Zb 12:6
Zb 119:160

c Zb 119:97

d Zb 22:6, 7

e Zb 36:6

f Kut 34:6
Zb 119:160
Yoh 17:17

g Zb 119:34

h Zb 5:3
Zb 88:13
Mk 1:35

i Zb 63:6
Lu 6:12

j Zb 51:1
Isa 63:7

Safu ya 2

a Kum 4:7
Zb 46:1
Zb 145:18

b Zb 19:9
Yoh 17:17

c Zb 119:144
Mhu 3:14

d Zb 9:13

e 1Sa 24:15
Zb 43:1

f 2Fa 17:15, 18
Zb 73:27
Met 15:29

g 1Nya 21:13
Zb 86:15
Isa 55:7
2Ko 1:3
Yak 5:11

h Zb 25:19

i Zb 139:21

j Zb 119:40, 88
Omb 3:22

150 Watu wenye mwenendo
wa aibu* hunikaribia;
Wako mbali sana na she-
ria yako.

151 Wewe uko karibu nami,
Ee Yehova,^a
Na amri zako zote ni
kweli.^b

152 Zamani za kale nilijifu-
nza kuhusu vikumbusho
vyako,
Ambavyo umeviweka
vidumu milele.^c

𐤒 [Resh]

153 Yatazame mateso yangu
na uniokoe,^d
Kwa maana sijaisahau
sheria yako.

154 Nitetee* na uniokoe;^e
Nihifadhi hai kulingana
na ahadi yako.[#]

155 Wokovu uko mbali sana
na waovu,
Kwa maana hawajayata-
futa masharti yako.^f

156 Rehema zako ni nyingi,
Ee Yehova,^g
Nihifadhi hai kulingana
na haki yako.

157 Wanaonitesa na pia maa-
dui wangu ni wengi;^h
Lakini sijakengeuka ku-
toka katika vikumbusho
vyako.

158 Ninawatazama wenye hila
kwa chuki kali,
Kwa sababu hawalishiki
neno lako.ⁱ

159 Tazama jinsi ninavyoya-
penda sana maagizo
yako!
Ee Yehova, nihifadhi hai
kwa sababu ya upendo
wako mshikamanifu.^j

119:150 *Au "mwenendo mpotovu."
119:154 *Au "lendeshe kesi yangu."
#Au "neno lako."

160 Kiini hasa cha neno lako ni kweli,^a
Na hukumu zako zote za uadilifu zinadumu milele.

𐤑 [Sin] au [Shin]

161 Wakuu wananitesa^b bila sababu,

Lakini moyo wangu unayahofu maneno yako.^c

162 Ninashangilia kwa sababu ya neno lako^d

Kama mtu anayepata nyara nyingi.

163 Nauchukia uwongo—nauchukia sana^e—

Ninaipenda sheria yako.^f

164 Mara saba kwa siku nina kusifu wewe

Kwa sababu ya hukumu zako za uadilifu.

165 Wale wanaoipenda sheria yako wana amani nyingi;^g

Hakuna chochote kinachoweza kuwakwaza.*

166 Ninayatazia matendo yako ya wokovu, Ee Yehova,

Nami ninazishika amri zako.

167 Ninavishika vikumbusho vyako,

Nami navipenda sana.^h

168 Ninayatii maagizo yako na vikumbusho vyako,

Kwa maana unajua mambo yote nina-yotenda.ⁱ

𐤍 [Taw]

169 Kilio changu cha kuomba msaada na kikufikie wewe, Ee Yehova.^j

Nifanye nielewe, kulingana na neno lako.^k

119:165 *Au "Hakuna cha kuwakwaza."

SURA YA 119

a 2Sa 7:28
Zb 12:6
Yoh 17:17

b Zb 119:23

c 2Fa 22:19

d Yer 15:16

e Zb 101:7
Zb 119:29, 104

f Zb 1:2

g Zb 1:2, 3
Met 3:1, 2
Isa 32:17
Isa 48:18

h Zb 1:2
Zb 40:8
Ro 7:22

i Zb 139:3
Met 5:21
Met 15:11
Ebr 4:13

j Zb 18:6

k 1Nya 22:12
Met 2:3, 5

Safu ya 2

a Zb 63:5
Zb 71:17
Zb 145:7

b Zb 40:9

c Zb 60:5

d Kum 30:19
Yos 24:15, 22

e Zb 1:2

f Zb 9:13, 14
Isa 38:19

g Zb 95:7
Lu 15:4
1Pe 2:25

h Mhu 12:13

SURA YA 120

i Zb 18:6

j Zb 50:15
Yon 2:1, 2

k Met 12:22

170 Ombi langu la kutaka kibalali na lifike mbele zako.

Niokoe, kama ulivyoa-hidi.*

171 Midomo yangu na ifurikwe na sifa,^a

Kwa maana wewe hunifundisha masharti yako.

172 Ulimi wangu na uimbe kuhusu neno lako,^b

Kwa maana amri zako zote ni za uadilifu.

173 Mkono wako na uwe tayari kunisaidia,^c

Kwa sababu nimechagua kutii maagizo yako.^d

174 Ninautamani sana wokuvu wako, Ee Yehova,

Nami ninaipenda sana sheria yako.^e

175 Acha niishi ili nikusifu;^f
Hukumu zako na ziwe msaada wangu.

176 Nimetangatanga kama kondoo aliyepotea,^g Nitafute mimi mtumishi wako,

Kwa maana sijazisahau amri zako.^h

Wimbo wa Safari za Kupanda.*

120 Nilimwita Yehova nilipokuwa nikitaa-bika,ⁱ

Naye akanijibu.^j

2 Ee Yehova, niokoe kutoka kwa midomo inayosema uwongo

Na kutoka kwa ulimi mdanganyifu.

3 Mungu atakufanya nini, Naye atakuadhibu jinsigani,*

Ewe ulimi mdanganyifu?^k

119:170 *Au "kulingana na neno lako."

120:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.

120:3 *Tnn., "Naye atakuongezea nini?"

4 Kwa mishale mikali^a ya shujaa

Na makaa yanayowaka moto^b ya miretemu.

5 Ole wangu, kwa maana nimeishi kama mgeni Mesheki!^c

Nimekuwa nikiishi kati ya mahema ya Kedari.^d

6 Nimekuwa nikiishi mbali kwa muda mrefu Pamoja na watu wanao-chukia amani.^e

7 Mimi ni mtu wa amani, lakini ninapooonga, Wao wanataka vita.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

121 Ninayainua macho yangu nitazame milimani.^f

Msaada wangu utatoka wapi?

2 Msaada wangu hutoka kwa Yehova,^g

Muumba wa mbingu na dunia.

3 Hataruhusu kamwe mguu wako uteleze.^{*h}

Yeye anayekulinda hatasinzia kamwe.

4 Tazama! Hatazinzia kamwe wala kulala usingizi,

Yeye anayelinda Israeli.ⁱ

5 Yehova anakulinda. Yehova ni kivuli/ kwenye mkono wako wa kulia.^k

6 Mchana, jua halitakucho- ma,^l

Wala mwezi usiku.^m

7 Yehova atakulinda dhidi ya madhara yote.ⁿ

Ataulinda uhai wako.^{*o}

8 Yehova atakulinda

SURA YA 120

a Zb 7:13

b Zb 140:10

c Mwa 10:2

d Yer 49:28

e Zb 57:4

SURA YA 121

f Zb 125:2

g Zb 46:1

Isa 41:13

Yer 20:11

Ebr 13:6

h Zb 91:11, 12

Met 3:26

i Isa 27:3

Isa 40:28

j Zb 91:1

Isa 25:4

k Zb 16:8

Zb 109:31

l Isa 49:10

Ufu 7:16

m Zb 91:5, 6

n Zb 91:10

Met 12:21

o Zb 97:10

Zb 145:20

Safu ya 2

SURA YA 122

a 2Sa 6:15

Zb 27:4

Zb 42:4

Zb 84:10

b 2Nya 6:6

Zb 84:7

Zb 100:4

c 2Sa 5:9

d Kut 23:17

Kum 12:5, 6

e Kum 17:8, 9

2Nya 19:8

f 2Sa 7:16

1Fa 10:18

1Nya 29:23

g Zb 51:18

katika mambo yote una- yofanya*

Kuanzia sasa mpaka milele.

Wimbo wa Safari za Kupanda. Wa Daudi.

122 Nilishangilia walipo- niambia:

“Na twende katika nyumba ya Yehova.”^a

2 Na sasa miguu yetu imesi- mama

Ndani ya malango yako, Ee Yerusalemu.^b

3 Yerusalemu limejengwa kama jiji

Ambalo limeunganishwa pamoja kama kitu kimoja.^c

4 Makabila yamepanda kwe- nda humo,

Makabila ya Yah,^{*}

Kulingana na kikumbusho walichopewa Waisraeli, Ili walishukuru jina la Ye- hova.^d

5 Kwa maana viti vya ufalme vya hukumu viliwekwa huko,^e

Viti vya ufalme vya nyu- mba ya Daudi.^f

6 Ombeni ili Yerusalemu liwe na amani.^g

Wale wanaokupenda, Ee jiji, watakuwa salama.

7 Amani na idumu ndani ya maboma yako,^{*}

Usalama ndani ya minara yako yenye ngome.

8 Kwa ajili ya ndugu zangu na rafiki zangu ni- tasema:

“Amani na iwe ndani yako.”

121:8 *Tnn., “unapotoka nje na unapoi- ngia ndani.” **122:4** *Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. **122:7** *Au “kuta zako zenye ngome.”

121:3 *Au “uyumbe.” 121:7 *Au “Atai- linda nafsi yako.”

- 9 Kwa ajili ya nyumba ya Yehova Mungu wetu,^a Nitakutakia mema.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

123

Nayainua macho yangu kukuelekea wewe,^b

Wewe unayeketi kwenye kiti cha ufalme mbinguni.

- 2 Kama macho ya watu-mishi yanavyoutazama mkono wa bwana wao, Na macho ya kijakazi yanavyoutazama mkono wa bimbubwa wake, Ndivyo macho yetu yanavyokutazama wewe, Ee Yehova Mungu wetu^c Mpaka utakapotuonyesha kibali.^d
- 3 Tuonyeshe kibali, Ee Yehova, tuonyeshe kibali, Kwa maana tumedharauliwa vya kutosha.^e
- 4 Tumedhihakiwa vya kutosha na* watu wanaojitumaini Na kudharauliwa na wenye kiburi.

Wimbo wa Safari za Kupanda. Wa Daudi.

124

“Kama Yehova hangekuwa pamoja nasi”^f

—Watu wa Israeli na wame sasa—

- 2 “Kama Yehova hangekuwa pamoja nasi^g Watu walipokuja kutushambulia,^h
- 3 Basi wangetumeza tukiwa haiⁱ Hasira yao ilipokuwa ikiwaka dhidi yetu.^j

123:4 *Au “Nafsi yetu imechoshwa na dhihaka nyingi za.”

SURA YA 122

a 1Nya 29:3
Zb 26:8
Zb 69:9

SURA YA 123

b Zb 25:15
Zb 121:1

c Zb 119:82
Zb 130:6

d Omb 3:25
Mik 7:7

e Ne 4:4
Zb 44:13

SURA YA 124

f Zb 46:7
Ro 8:31
Ebr 13:6

g Zb 54:4
Zb 118:6

h Zb 3:1
Zb 22:16

i Zb 27:2

j Zb 56:1

Safu ya 2

a Zb 18:4

b 1Sa 23:26-28
2Sa 17:21, 22

c Zb 25:15
Zb 91:3

d Met 18:10

SURA YA 125

e Yer 17:7

f 1Fa 8:12, 13
Zb 48:2
Zb 132:13, 14

g 1Fa 11:7
Mdo 1:12

h Zb 34:7
Isa 31:5
Zek 2:4, 5

i Isa 14:5

j Mhu 7:7

k Zb 51:18

l Zb 36:10
Zb 73:1

- 4 Kisha maji yangetufagilia mbali, Mafuriko yangetufunika.^a
- 5 Maji yenye nguvu yangetulemea.
- 6 Yehova na asifiwe, Kwa maana hakututia katika meno yao kama mawindo.
- 7 Sisi* ni kama ndege aliyeponyoka Kutoka katika mtego wa mwindaji;^b Mtego ulivunjika, Nasi tukaponyoka.^c
- 8 Msaada wetu uko katika jina la Yehova,^d Muumba wa mbingu na dunia.”

Wimbo wa Safari za Kupanda.

125

Wale wanaomtumaini Yehova^e

Ni kama Mlima Sayuni, ambao hauwezi kutikiswa

Bali hudumu milele.^f

- 2 Kama milima inavyozunguka Yerusalemu,^g Ndivyo Yehova anavyowazunguka watu wake^h Kuanzia sasa mpaka milele.
- 3 Fimbo ya ufalme ya uovu haitadumu katika nchi waliyogawiwa waadilifu,ⁱ Ili waadilifu wasije wakatenda* jambo baya.^j
- 4 Ee Yehova, watendee mema walio wema,^k Walio wanyoofu moyoni mwao.^l
- 5 Lakini wale wanaogeuka na kufuata njia zao zilizopotoka,

124:7 *Au “Nafsi yetu.” 125:3 *Au “wasielekeze mikono yao kutenda.”

Yehova atawaondoa pamoja na watenda maovu.^a
Amani na iwe juu ya Israeli.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

126 Yehova alipowakusanya na kuwarudisha mateka wa Sayuni,^b

Tulifikiri tunaota ndoto.

2 Wakati huo kinywa chetu kilijaa kicheko Na ulimi wetu kelele za shangwe.^c

Wakati huo ilisemwa miongoni mwa mataifa: “Yehova amewatendea mambo makuu.”^d

3 Yehova ametutendea mambo makuu,^e Nasi tuna shangwe nyingi sana.

4 Wakusanye na kuwarudisha watu wetu waliotekwa, Ee Yehova, Kama vijito vya Negebu.*

5 Wale wanaopanda mbegu kwa machozi Watavuna kwa kelele za shangwe.

6 Yule anayetoka kwenda nje, ingawa analia, Akiwa amebeba mfuko wake uliojaa mbegu, Kwa hakika atarudi kwa kelele za shangwe,^f Akiwa amebeba masuke yake.^g

Wimbo wa Safari za Kupanda. Wa Sulemani.

127 Yehova asipoijenga nyumba, Wale wanaoijenga wanafanya kazi ngumu ya bure.^h

SURA YA 125

a 1Nya 10:13
Zb 53:5
Isa 59:8

SURA YA 126

b Ezz 1:2, 3
Zb 85:1

c Ezz 3:11
Zb 106:47
Isa 49:13
Yer 31:12

d Yos 2:9, 10
Ne 6:15, 16

e Ezz 7:27, 28
Isa 11:11

f Zb 30:5
Isa 61:1-3

g Isa 9:3

SURA YA 127

h Met 3:6
Met 10:22
Met 16:3

Safu ya 2

a Isa 27:3

b Zb 3:5
Mhu 5:12

c Mwa 33:4, 5
Mwa 48:3, 4
1Sa 2:21

d Mwa 41:51, 52
Law 26:9
Ayu 42:12, 13
Zb 128:3

e Met 17:6

f Mwa 50:23

SURA YA 128

g Zb 112:1
Ebr 5:7

h Zb 119:1
Mik 6:8

i Mhu 5:18
Isa 65:22

j Kut 23:26
Zb 127:3

Yehova asipolilinda jiji,^a
Mlinzi anakesha bure.

2 Mnajisumbua bure kuumka mapema, Na kuchelewa kulala, Mkitaabika kupata chakula,

Kwa maana yeye huwaandalia anaowapenda na kuwapa usingizi.^b

3 Tazama! Watoto* ni urithi kutoka kwa Yehova;^c Uzao wa tumbo ni thawabu.^d

4 Kama mishale mkononi mwa mwanamume hodari, Ndivyo walivyo watoto ambao mtu anawazaa akiwa kijana.^e

5 Mwenye furaha ni mwanamume anayelijaza podo lake watoto.^f Hawataaibishwa, Kwa maana watazungumza na maadui katika lango la jiji.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

128 Mwenye furaha ni kila mtu anayemwogopa Yehova,^g

Anayetembea katika njia Zake.^h

2 Utakula mazao ambayo mkono wako ulifanya kazi ngumu kuyapata.

Utakuwa na furaha na kufurahia ufanisi.ⁱ

3 Mke wako atakuwa kama mzabibu unaozaa matunda mengi nyumbani mwako;^j

Watoto wako watakuwa kama machipukizi ya mzeituni kuzunguka meza yako.

127:3 *Au “Wana.”

126:4 *Au “makorongo ya kusini.”

- 4 Tazama! Hivyo ndivyo mwanamume anayemwogopa Yehova Atakavyobarikiwa.^a
- 5 Yehova atakubariki kutoka Sayuni. Na uone Yerusalemu likipata ufansi sikuzote za maisha yako^b
- 6 Na uone watoto wa watoto wako. Na amani iwe juu ya Israeli.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

129 “Wamenishambulia daima tangu nilipokuwa kijana”^c

—Watu wa Israeli na wame sasa—

- 2 “Wamenishambulia daima tangu nilipokuwa kijana;^d Lakini hawajanishinda.^e
- 3 Wale wanaolima kwa jembe la plau wamelima mgongoni mwangu;^f Wameirefusha mitaro yao.”
- 4 Lakini Yehova ni mwadilifu;^g Amezikatakata kamba za waovu.^h
- 5 Wataaibishwa na kukiambia kwa fedheha, Wale wote wanaolichukia Sayuni.ⁱ
- 6 Watakuwa kama majani juu ya paa Yanayonyauka kabla haya-
jang’olewa,
- 7 Ambayo hayawezi kujaa mkononi mwa mvunaji Wala mikononi mwa yule anayekusanya masuke.
- 8 Wale wanaopita karibu nao hawatasesa: “Baraka ya Yehova na iwe juu yenu;

SURA YA 128

a Zb 127:4, 5

b Zb 122:6
Isa 33:20

SURA YA 129

c Kut 5:6, 9

d Omb 1:3

e Zb 118:13
Zb 125:3

f Zb 66:12
Isa 51:23

g Ezz 9:15
Ne 9:33

h Zb 124:7

i Ne 4:4
Ne 6:15, 16
Est 6:13
Est 9:5
Zb 137:7
Zek 12:3

Safu ya 2

SURA YA 130

a Omb 3:55
Yon 2:1, 2

b Zb 38:4
Zb 103:14
Zb 143:1, 2
Isa 55:7
Da 9:18
Ro 3:20
Tit 3:5

c Kut 34:6, 7
Zb 25:11

d Yer 33:8, 9

e Mik 7:7

f Zb 119:147

g Zb 86:5

SURA YA 131

h Zb 78:70
Zb 138:6

Tunawabariki katika jina la Yehova.”

Wimbo wa Safari za Kupanda.

130 Kutoka vilindini ninakulilia, Ee Yehova.^a

- 2 Ee Yehova, isikie sauti yangu. Masikio yako na yasikilize sihi zangu za kuomba msaada.
- 3 Ikiwa ungekuwa unatazama* tu makosa, Ee Yah,[#] Basi ni nani, Ee Yehova, angeweza kusimama?^b
- 4 Kwa maana wewe hutoa msamaha wa kweli,^c Ili watu wakuhofu.*^d
- 5 Ninamtumaini Yehova, nafsi yangu yote inamtumaini; Ninangoja neno lake.
- 6 Ninamngojea Yehova kwa hamu,^e Kuliko walinzi wanavyoiingojea asubuhi,^f Naam, kuliko walinzi wanavyoingojea asubuhi.
- 7 Watu wa Israeli na waendeleo kumngojea Yehova, Kwa maana Yehova ni mshikamanifu katika upendo wake,^g Naye ana nguvu nyingi za kukomboa.
- 8 Atawakomboa watu wa Israeli kutoka katika makosa yao yote.

Wimbo wa Safari za Kupanda. Wa Daudi.

131 Ee Yehova, moyo wangu hauna kiburi, Wala macho yangu hayana majivuno;^h

130:3 *Au “unafuatilia.” #“Yah” ni ufu-pisho wa jina Yehova. 130:4 *Tnn., “Ili uogopwe.”

Wala sijitafutii mambo makubwa sana,^a

Wala mambo yanayopita uwezo wangu.

- 2 Hasha, badala yake nimeituzia na kuinyamazisha nafsi yangu^{*b}

Kama mtoto aliyeachishwa kunyonya aliye na mama yake;

Nimeridhika kama mtoto aliyeachishwa kunyonya.

- 3 Watu wa Israeli na wamngojee Yehova^c
Kuanzia sasa mpaka milele.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

132 Ee Yehova, mkumbu-ke Daudi

Na mateso yake yote;^d

- 2 Jinsi alivyomwambia Yehova,

Jinsi alivyomwekea nadhiri hii Mwenye Nguvu wa Yakobo;^e

- 3 "Sitaingia katika hema langu, nyumbani mwangu.^f

Sitalala kwenye kochi langu, kitandani mwangu;

- 4 Sitayaruhusu macho yangu yalale usingizi, Wala kope zangu kusinzia

- 5 Mpaka nitakapopata mahali kwa ajili ya Yehova, Makao bora^{*} kwa ajili ya Mwenye Nguvu wa Yakobo."^g

- 6 Tazama! Tulisikia habari hizo huko Efratha;^h
Tulizipata katika masha-mba yaliyo msituni.ⁱ

131:2 *Au "nimejituliza na kujinyamazisha mwenyewe." Angalia Kamusi, uku. 2012. 132:5 *Au "Hema tukufu la ibada."

SURA YA 131

a 1Sa 18:23

b 1Sa 30:6
Zb 62:1
Isa 30:15
Omb 3:26

c Zb 130:7
Mik 7:7

SURA YA 132

d 1Sa 20:1

e 2Sa 7:2, 3

f 2Sa 5:11

g 2Sa 7:2
1Fa 8:17
1Nya 15:3, 12
Mdo 7:45, 46

h 1Sa 17:12

i 1Sa 7:1
1Nya 13:6

Safu ya 2

a Zb 43:3

b 1Nya 28:2
Zb 5:7

c Hes 10:35
2Sa 6:17

d 2Nya 6:41, 42

e 1Fa 15:4
2Fa 19:34

f 1Fa 8:25
Zb 89:3, 4
Zb 89:20, 36
Isa 9:7
Yer 33:20, 21
Mt 9:27
Lu 1:69
Mdo 2:30, 31
Mdo 13:22, 23

g 1Nya 29:19

h 2Sa 7:12, 16
1Nya 17:11, 12
Zb 89:20, 29

i Zb 48:2, 3
Zb 78:68
Ebr 12:22

j Zb 87:2

k Zb 46:5
Isa 24:23

- 7 Na tuingie katika makao yake;^{*a}

Na tuiname chini kwenye kiti cha miguu yake.^b

- 8 Inuka, Ee Yehova, uje mahali pako pa kupumzikia,^c

Wewe na Sanduku la nguvu zako.^d

- 9 Makuhani wako na wavae uadilifu, Washikamanifu wako na wapaze sauti kwa shangwe.

- 10 Kwa ajili ya Daudi mtumishi wako, Usimkatae^{*} mtiwa-mafuta wako.^e

- 11 Yehova amemwambia Daudi;

Kwa hakika hatakosa kutimiza neno lake:

"Mmoja wa wazao wako,^{*} Nitamfanya aketi kwenye kiti chako cha ufalme.^f

- 12 Wana wako wakilishika agano langu

Na vikumbusho vyangu ni navyowafundisha,^g

Wana wao pia

Wataketi kwenye kiti chako cha ufalme milele."^h

- 13 Kwa maana Yehova amelichagua Sayuni;ⁱ
Amelitamani liwe makao yake!^j

- 14 "Hapa ndipo mahali pangu pa kupumzikia milele;

Nitakaa hapa,^k kwa maana nimepatamani.

- 15 Nitapabariki sana kwa vyakula;

132:7 *Au "hema lake tukufu la ibada." 132:10 *Tnn., "Usiugeuze nyuma uso wa." 132:11 *Tnn., "Mmoja kutoka katika uzao wa tumbo lako."

Nitawashibisha maskini wake kwa mikate.^a

16 Makuhani wake nitawavisha wokovu,^b

Na washikamanifu wake watapaza sauti kwa shangwe.^c

17 Huko nitazifanya nguvu za Daudi zikue.*

Nimemtayarishia taa mtiwa-mafuta wangu.^d

18 Nitawavisha aibu maadui wake, Lakini taji lililo kwenye kichwa chake litasitawi.”^e

Wimbo wa Safari za Kupanda. Wa Daudi.

133 Tazama! Jinsi ilivyo vema na jinsi inavyopendeza

Ndugu kukaa pamoja kwa umoja!^f

2 Ni kama mafuta bora yanayomiminwa kichwani^g Yanayotiririka kwenye ndevu,

Ndevu za Haruni,^h Na kutiririka mpaka kwenye ukosi wa mavazi yake.

3 Ni kama umande wa Hermoniⁱ

Unaoshuka kwenye milima ya Sayuni.^j

Huko ndiko Yehova alikoamuru baraka yake —Uzima wa milele.

Wimbo wa Safari za Kupanda.

134 Msifuni Yehova, Enyi nyote watumishi wa Yehova,^k

Ninyi mnaosimama katika nyumba ya Yehova nyakati za usiku.^l

132:17 *Tnn., “nitaifanya pembe ya Daudi ikue.”

SURA YA 132

a Zb 22:26
Zb 147:12, 14

b Zb 149:4

c Zb 132:8, 9

d 1Fa 11:36
1Fa 15:4
2Nya 21:7

e Zb 2:6
Zb 72:8
Isa 9:6
Ufu 11:15

SURA YA 133

f Mwa 13:8
Yoh 13:35
Kol 3:14
Ebr 13:1

g Met 27:9

h Kut 29:4, 7

i Kum 3:8, 9
1Nya 5:23

j Zb 125:2

SURA YA 134

k Ufu 19:5

l 1Nya 9:33
1Nya 23:27, 30
Lu 2:37
Ufu 7:15

Safu ya 2

a Zb 28:2
Zb 141:2

SURA YA 135

b Zb 113:1
Ufu 19:5

c Zb 96:8
Zb 116:19

d Zb 119:68
Mt 19:17

e Kut 19:5
Kum 7:6

f Kum 10:17
Zb 97:9

g Zb 115:3
Isa 46:10

2 Inueni mikono yenu^a kati-ka utakatifu*^a

Na mumsifu Yehova.

3 Yehova, Muumba wa mbingu na dunia, Na awabariki kutoka Sayuni.

135 Msifuni Yah!^a Lisifuni jina la Yehova;

Msifuni, enyi watumishi wa Yehova,^b

2 Ninyi mnaosimama katika nyumba ya Yehova, Katika nyua za nyumba ya Mungu wetu.^c

3 Msifuni Yah, kwa maana Yehova ni mwema.^d Liimbieni sifa* jina lake, kwa maana linapendeza.

4 Kwa maana Yah amemchagua Yakobo kwa ajili yake mwenyewe, Israeli awe mali yake ya pekee.*^e

5 Kwa maana ninajua vizuri kwamba Yehova ni mkuu; Bwana wetu ni mkuu kuliko miungu mingine yote.^f

6 Yehova hufanya kila jambo apendalo^g Mbinguni na duniani, baharini na katika vilindi vyote.

7 Huyafanya mawingu yampande* kutoka kwenye miisho ya dunia; Hutengeneza radi^h kwa ajili ya mvua;

134:2 *Au labda, “mahali patakatifu.” 135:1 *Au “Haleluya!” “Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. 135:3 *Au “Lipigieni muziki.” 135:4 *Au “mali yake anayothamini sana.” 135:7 *Au “Huufanya mvuke upande.” #Au labda, “malango.”

Huutoa upepo katika ma-
ghala yake.^a

8 Aliwaua wazaliwa wa kwa-
nza wa Misri,
Wanadamu na wanyama
pia.^b

9 Alipeleka ishara na miuji-
kati kati yako, Ee Misri,^c
Dhidi ya Farao na watumi-
shi wake wote.^d

10 Aliyaangamiza mataifa
mengi^e
Na kuwaua wafalme ho-
dari^f

11 –Sihoni mfalme wa Waa-
mori,^g
Ogu mfalme wa Bashani,^h
Na falme zote za Kanaani.

12 Aliitoe nchi yao kuwa uri-
thi,
Urithi kwa watu wake Wa-
israeli.ⁱ

13 Ee Yehova, jina lako lina-
dumu milele.
Ee Yehova, umaarufu wako
unadumu* katika vizazi
vyote.^j

14 Kwa maana Yehova atawa-
tetea* watu wake,^k
Naye atawahurumia* wa-
tumishi wake.^l

15 Sanamu za mataifa ni fe-
dha na dhahabu,
Kazi ya mikono ya mwana-
damu.^m

16 Zina kinywa, lakini hazi-
wezi kuongea;ⁿ
Zina macho, lakini haziwe-
zi kuona;

17 Zina masikio, lakini hazi-
wezi kusikia.
Hazina pumzi vinywani
mwake.^o

135:13 *Au "jina lako linadumu." Tnn.,
"ukumbusho wako unadumu." 135:14
*Au "ataamua kesi ya." #Au "ataghairi
kuwahusu."

SURA YA 135

a Kut 14:21
Hes 11:31
Yer 10:13
Yer 51:16
Yon 1:4

b Kut 12:12, 29

c Kut 7:20
Kut 8:6, 17
Kut 9:6, 10
Kut 9:23
Kut 10:12, 21

d Zb 136:15

e Zb 44:2

f Yos 12:7, 8

g Hes 21:23, 24

h Hes 21:33-35

i Yos 11:23

j Kut 3:15
Zb 102:12

k Kut 14:31

l Kum 32:36

m Zb 115:4-8

Isa 46:6

Mdo 17:29

1Ko 10:19

n Hab 2:19

o Yer 10:14

Safu ya 2

a Isa 44:9

b Zb 97:7

c Kum 10:8

d Zb 48:1

Zb 132:13

e Yer 3:17

f Ufu 19:6

SURA YA 136

g Lu 18:19

h 2Nya 7:3

2Nya 20:21

Zb 106:1

Zb 107:1

i Zb 97:9

Da 2:47

j Kut 15:11

Ufu 15:3

k Zb 103:17

l Ayu 38:36

Met 3:19, 20

18 Watu wanaozitengeneza
watakuwa kama sanamu
hizo,^a

Na pia wote wanaozitu-
maini.^b

19 Ee nyumba ya Israeli,
msifuni Yehova.

Ee nyumba ya Haruni,
msifuni Yehova.

20 Ee nyumba ya Lawi,
msifuni Yehova.^c

Enyi mnaomwogopa
Yehova, msifuni
Yehova.

21 Yehova na asifiwe kutoka
Sayuni,^d

Yeye anayekaa Yerusa-
lemu.^e

Msfuni Yah!^f

136 Mshukuruni Yehova,
kwa maana ni
mwema;^g

Upendo wake mshikamani-
fu unadumu milele.^h

2 Mshukuruni Mungu wa
miungu,ⁱ

Kwa maana upendo wake
mshikamanifu unadumu
milele.

3 Mshukuruni Bwana wa
mabwana,

Kwa maana upendo wake
mshikamanifu unadumu
milele.

4 Yeye peke yake ndiye
anayetenda mambo
makuu yanayostaaja-
bisha,^j

Kwa maana upendo wake
mshikamanifu unadumu
milele.^k

5 Aliziumba mbingu kwa
ustadi,^{*l}

Kwa maana upendo wake
mshikamanifu unadumu
milele.

136:5 *Au "kwa uelewaji."

- 6** Aliitandaza dunia juu ya maji,^a
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 7** Aliiumba ile mianga mi-kubwa,^b
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele,
- 8** Jua litawale mchana,^c
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele,
- 9** Mwezi na nyota zitawale usiku,^d
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 10** Aliwaua wazaliwa wa kwanza wa Misri,^e
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 11** Aliwatoa Waisraeli kutoka kati yao,^f
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele,
- 12** Kwa mkono wenye nguvu^g na mkono ulionyooshwa,
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 13** Aliigawa Bahari Nyekundu sehemu mbili,^{*h}
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 14** Aliwavusha Waisraeli kati-kati yake,ⁱ
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 15** Alimkung'uta Farao na jeshi lake ndani ya Bahari Nyekundu,^j

SURA YA 136

a Mwa 1:9
Zb 24:1, 2

b Mwa 1:14

c Mwa 1:16
Yer 31:35

d Zb 8:3

e Kut 12:29

f Kut 12:51

g Kut 13:14

h Kut 14:21

i Kut 14:29

j Kut 14:27, 28

Safu ya 2

a Kut 13:18
Kut 15:22

b Yos 12:7, 8

c Hes 21:21-24

d Hes 21:33-35

e Hes 32:33

f Kum 32:36

g Ne 9:32

h Amu 3:9
Amu 6:9

Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.

- 16** Aliwaongoza watu wake kupitia nyikani,^a
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 17** Aliwaua wafalme wakuu,^b
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 18** Aliwaua wafalme hodari,
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 19** Sihoni^c mfalme wa Waa-mori,
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele,
- 20** Na Ogu^d mfalme wa Bashani,
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 21** Aliitoa nchi yao kuwa urithi,^e
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 22** Urithi kwa Israeli mtumishi wake,
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.
- 23** Alitukumbuka tulipokuwa wanyonge,^f
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.^g
- 24** Alituokoa tena na tena kutoka kwa maadui wetu,^h
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.

25 Huwapa chakula viumbe wote walio hai,*^a
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.

26 Mshukuruni Mungu wa mbinguni,
Kwa maana upendo wake mshikamanifu unadumu milele.

137 Kando ya mito ya Babiloni,^b hapo ndipo tulipoketi.

Tulilia tulipokumbuka Sayuni.^c

2 Juu ya miti ya mierebi iliyo ndani yake,*

Tulitundika vinubi vyetu.^d

3 Kwa maana huko, walio-tuteka walitaka tuwaimbie,^e

Waliotudhahiki walitaka tuwatumbuize:

“Tuimbieni mojawapo ya nyimbo za Sayuni.”

4 Tunawezaje kuimba wimbo wa Yehova

Katika nchi ya kigeni?

5 Ikiwa nitakusahau wewe, Ee Yerusalemu,
Mkono wangu wa kulia na uwe msahaulifu.*^f

6 Ulimi wangu na ushikamane na kaaka langu Nisipokukumbuka, Nisipoliweka Yerusalemu juu ya

Sababu zangu kuu zaidi za kushangilia.^g

7 Kumbuka, Ee Yehova, Mambo ambayo Waedomu walisema siku ambayo Yerusalemu lilianguka: “Libomoeni! Libomoeni

136:25 *Tnn., “Huipa chakula miili yote.” 137:2 *Yaani, Babiloni. 137:5 *Au labda, “unyauke.”

SURA YA 136

a Zb 145:15
Zb 147:9

SURA YA 137

b Yer 51:13
Eze 3:15
Da 10:4

c Da 9:2, 3

d Isa 24:8

e Zb 123:4

f Ne 2:3
Zb 84:2
Zb 102:13, 14
Isa 62:1
Yer 51:50

g Zb 122:1

Safu ya 2

a Yer 49:7
Omb 4:22
Eze 25:12
Oba 10-13

b Isa 47:1
Yer 25:12
Yer 50:2

c Yer 50:29
Ufu 18:6

d Isa 13:1, 16

SURA YA 138

e Zb 9:1

f Isa 3:3
1Nya 16:1
Zb 28:2

g Yoh 17:6

h Zb 18:6

i Zb 29:11
Isa 12:2
Isa 41:10

j Zb 102:15
Isa 60:3

k 1Fa 8:10, 11

mpaka kwenye misingi yake!”^a

8 Ee binti ya Babiloni, uliye karibu kuangamizwa,^b
Mwenye furaha ni yule atakayekupa thawabu yako

Kwa maovu uliyotutendea.^c

9 Mwenye furaha ni yule atakayewakamata kwa nguvu watoto wako
Na kuwafunda juu ya miamba.^d

Wa Daudi.

138 Nitakusifu kwa moyo wangu wote.^e

Mbele ya miungu mingine, Nitaimba sifa.*

2 Nitainama chini kuelekea hekalu lako takatifu,*^f

Nami nitalisifu jina lako^g

Kwa sababu ya upendo wako mshikamanifu na uaminifu wako.

Kwa maana umelitukuza neno lako na jina lako juu ya vitu vingine vyote.^h

3 Siku niliyokuita, ulinijibu;^h
Ulinifanya niwe jasiri* na mwenye nguvu.ⁱ

4 Wafalme wote wa dunia watakusifu wewe, Ee Yehova,^j

Kwa maana watakuwa wamesikia ahadi ulizotoa.

5 Wataimba kuhusu njia za Yehova,
Kwa maana utukufu wa Yehova ni mkuu.^k

138:1 *Au labda, “Nitaipinga miungu mingine kwa kukupigia muziki.” 138:2 *Au “mahali pake patakatifu.” ^aAu labda, “umelitukuza neno lako juu ya jina lako lote.” 138:3 *Au “niwe na ujasiri katika nafsi yangu.”

6 Ingawa Yehova yuko juu,
yeye huwaona wanyenye-
kevu,^a

Lakini anajitenga mbali na
wenye kiburi.^b

7 Hata nikitembea katikati
ya hatari, utanihifadhi
hai.^c

Unaunyoosha mkono
wako dhidi ya hasira ya
maadui wangu;

Mkono wako wa kuume
utaniokoa.

8 Yehova atayatimiza
mambo yote kwa niaba
yangu.

Ee Yehova, upendo wako
mshikamanifu unadumu
milele;^d

Usiziache kazi za mikono
yako.^e

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

139 Ee Yehova, umeni-
chunguza kabisa,
nawe unanijua.^f

2 Unajua wakati ninapoketi
na wakati ninaposi-
mama.^g

Unatambua mawazo yangu
kutoka mbali.^h

3 Unanichunguza* ninapo-
safiri na ninapolala;
Unazijua njia zangu zote.ⁱ

4 Kabla sijatamka neno lolo-
te kwa ulimi wangu,
Tazama! Ee Yehova, tayari
unalijua vizuri.^j

5 Unanizingira nyuma na
mbele;

Nawe unauweka mkono
wako juu yangu.

6 Ujuzi huo unazidi ufaha-
mu wangu.*

Uko juu sana nisiweze kuu-
fikia.^{#k}

SURA YA 138

a 1Sa 2:8
Zb 113:6-8
Isa 57:15

b Yak 4:6
1Pe 5:5

c Zb 71:20

d Zb 103:17

e Ayu 14:15
Zb 71:18

SURA YA 139

f 1Sa 16:6, 7
1Nya 28:9
Zb 17:3
Zb 139:23
Yer 20:12

g Mwa 16:13

h Zb 94:11

i Mwa 28:15
2Sa 8:14
Ayu 31:4
Zb 121:8
Met 5:21

j Ebr 4:12

k Ayu 26:14
Ayu 42:3
Zb 40:5
Ro 11:33

Safu ya 2

a Yon 1:3

b Ayu 26:6
Met 15:11

c Zb 63:8
Zb 73:23
Isa 41:13

d Da 2:22

e Ebr 4:13

f Zb 22:9
Zb 71:6
Yer 1:5

g Mwa 1:26

h Zb 19:1
Zb 104:24
Zb 111:2
Ufu 15:3

7 Ninaweza kujificha wapi
mbali na roho yako,
Na ni wapi ninapoweza
kukimbia mbali na uso
wako?^a

8 Kama ningepanda mbi-
nguni, ungekuwa huko,
Na kama ningetandika
kitanda changu Kaburi-
ni,* tazama! ungekuwa
huko.^b

9 Kama ningeruka kwa ma-
bawa ya mapambazuko
Ili niishi kando ya bahari
iliyo mbali zaidi,

10 Hata huko mkono wako
ungeniongoza
Na mkono wako wa kuume
ungenishika.^c

11 Nikisema: "Hakika giza li-
tanificha!"
Basi usiku unaonizunguka
utakuwa nuru.

12 Hata giza halitakuwa zito
mno kwako,
Lakini usiku utakuwa
mwangavu kama
mchana;^d

Kwako giza ni sawa na
nuru.^e

13 Kwa maana uliziumba figo
zangu;
Ulinisitiri* katika tumbo la
mama yangu.^f

14 Ninakusifu kwa sababu
nimeumbwa kwa njia
inayoogopesha na
kustaajibisha.^g
Kazi zako zinastaajibisha,^h
Ninajua* vizuri sana
jambo hilo.

15 Mifupa yangu haikufichwa
kwako

139:8 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi,
uku. 2012. 139:13 *Au labda, "Ulinifu-
ma pamoja." 139:14 *Au "Nafsi yangu
inajua."

139:3 *Tnn., "Unanipima." 139:6 *Au
"ni wa ajabu sana kwangu." #Au "Ume-
zidi kabisa uelewaji wangu."

Nilipombwa sirini,
Nilipofumwa katika sehemu zenye kina za dunia.^a

16 Macho yako hata yaliniona nikiwa kiinitete;

Sehemu zake zote ziliandikwa katika kitabu chako Kuhusiana na siku ambazo zingeeumbwa,
Kabla sehemu yoyote haijakuwepo.

17 Kwa hiyo kwangu mimi, mawazo yako ni yenye thamani sana!^b

Ee Mungu, jinsi jumla yake ilivyo kubwa sana!^c

18 Nikijaribu kuyahesabu, ni mengi kuliko chembe za mchanga.^d

Nikiamka, bado nipo pamoja nawe.^{*e}

19 Ee Mungu, laiti ungewaua waovu!^f

Ndipo watu wakatili* wangeniondokea,

20 Wale wanaosema mambo mabaya kukuhusu kwa nia ovu;*

Wao ni maadui wako wanaolitumia jina lako kwa njia isiyofaa.^g

21 Je, siwachukii wale wanaokuchukia wewe, Ee Yehova,^h

Na kuwachukia kabisa wale wanaokuasi?!

22 Ninawachukia kwelikweli;/ Hakika wamekuwa maadui wangu.

23 Nichunguze kabisa, Ee Mungu, uujue moyo wangu.^k

Nipime, uyajue mawazo

139:18 *Au labda, "nitakuwa bado ninayahesabu." 139:19 *Au "wenye hatia ya damu." 139:20 *Au "kulingana na mawazo yao."

SURA YA 139

a Ayu 10:10, 11

b Isa 55:9

c Ro 11:33

d Zb 40:5

e Zb 63:6

f Zb 5:6

g Kut 20:7

h 2Nya 19:2
2Ko 6:14

i Zb 119:158

j Zb 101:3

k Yer 20:12

Safu ya 2

a Zb 94:19

b Zb 17:3

c Zb 5:8
Zb 143:8
Zb 143:10

SURA YA 140

d Zb 18:48
Zb 59:1

e Zb 64:2, 6

f Zb 52:1, 2
Zb 58:3, 4

g Ro 3:13
Yak 3:8

h Zb 17:8
Zb 36:11
Zb 71:4

i Zb 10:9

j Yer 18:22

k Zb 28:2
Zb 55:1

l 1Sa 17:37

yangu yanayonihangaisha.^{*a}

24 Angalia ikiwa kuna njia yoyote yenye madhara ndani yangu,^b

Uniongoze^c katika njia ya milele.

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

140 Niokoe, Ee Yehova, kutoka kwa watu waovu;

Nilinde kutoka kwa watu wakatili,^d

2 Wale wanaopanga njama za uovu mioyoni mwao^e Na kuchochea vita mchana kutwa.

3 Wanaunoa ulimi wao kama wa nyoka;^f Sumu ya nyoka vipiri iko nyuma ya midomo yao.^g (Sela)

4 Nilinde, Ee Yehova, kutoka mikononi mwa waovu;^h Nilinde kutoka kwa watu wakatili,

Wale wanaopanga njama ya kunitega miguu.

5 Wenye kiburi huuficha mtego ili uninase; Kwa kamba wanautandaza wavu kando ya njia.ⁱ Wanatega mitego ya kuni-nasa.^j (Sela)

6 Ninamwambia Yehova: "Wewe ni Mungu wangu. Sikiliza, Ee Yehova, sihi zangu za kuomba msaada."^k

7 Ee Yehova Bwana Mwenye Enzi Kuu, Mwokozi wangu mwenye nguvu, Wewe hukinga kichwa changu katika siku ya vita.^l

8 Ee Yehova, usitosheleze tamaa za waovu.

139:23 *Au "yanayonifadhaisha."

Usiruhusu njama zao zi-fanikiwe, ili wasijikweze. (Sela)^a

9 Vichwa vya wale wanaoningira

Na vifunikwe na uovu unaosemwa na midomo yao.^b

10 Makaa ya mawe yanayowaka na yawanyeshee kama mvua.^c

Na watupwe motoni, Ndani ya mashimo yenye kina,^{*d} wasiinuke tena kamwe.

11 Mchongezi na asipate makao duniani.^{*e}

Uovu na uwafuatie watu wakatili na kuwaangamiza.

12 Ninajua kwamba Yehova atawatetea watu wa hali ya chini

Na kuwatendea haki maskini.^f

13 Hakika waadilifu watalishukuru jina lako; Wanyoofu watakaa mbele za uso wako.^{*g}

Muziki wa Daudi.

141 Ee Yehova, ninakulia wewe.^h

Njoo haraka unisaidie.ⁱ Sikiliza ninapokulilia.^j

2 Sala yangu na itayarishwe kama uvumba^k mbele zako,^l

Mikono yangu iliyoinuliwa na iwe kama toleo la jioni la nafaka.^m

3 Weka mlinzi wa kinywa changu, Ee Yehova,

Weka ulinzi kwenye mlango wa midomo yangu.ⁿ

140:10 *Au "Mashimo yenye umajimaji." 140:11 *Au "nchini." 140:13 *Au "katika uwepo wako."

SURA YA 140

a 2Sa 15:31
Zb 27:12

b Zb 7:16
Met 12:13

c Zb 11:5, 6

d Zb 55:23

e Zb 12:3

f Zb 10:17, 18
Zb 22:24

g Zb 23:6

SURA YA 141

h Zb 31:17

i Zb 40:13
Zb 70:5

j Zb 39:12

k Kut 30:34-36

l Lu 1:9, 10
Ufu 5:8
Ufu 8:3, 4

m Kut 29:41

n Met 13:3
Met 21:23
Yak 1:26

Safu ya 2

a 1Fa 8:58
Zb 119:36

b 2Sa 12:7, 9
Met 17:10
Gal 6:1

c Met 6:23
Yak 5:14

d Met 9:8
Met 19:25
Met 25:12

e 2Nya 20:12
Zb 25:15

f Est 7:10
Zb 7:14, 15
Zb 9:15
Zb 57:6

4 Usiache moyo wangu uelekee kwenye jambo lolote ovu,^a

Nisishirikiane na watu waovu kutenda mambo mapotovu;

Nisile kamwe vyakula vyao vitamu.

5 Mwadilifu akinipiga, hilo litakuwa tendo la upe-ndo mshikamanifu;^b

Akinikaripia, hilo litakuwa kama mafuta kwenye kichwa changu,^c

Ambayo kichwa changu hakiwezi kamwe kukataa.^d

Nitaendelea kusali hata wanapopatwa na misiba.

6 Ingawa waamuzi wao wanatupwa chini kutoka kwenye jabali,

Watu watayasikiliza maneno yangu, kwa maana yanapendeza.

7 Kama mtu anavyolima na kuuvunja-vunja udongo,

Ndivyo mifupa yetu ilivyotawanywa kwenye mlango wa Kaburi.^{*}

8 Lakini macho yangu yanakutazama wewe, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.^e

Nimekukimbilia wewe. Usiniue.^{*}

9 Nilinde dhidi ya mataya ya mtego walionitegea, Dhidi ya mitego ya wate-nda maovu.

10 Waovu wote wataanguka pamoja ndani ya nyavu zao wenyewe^f

Huku nikipitia karibu nazo kwa usalama.

141:7 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 141:8 *Au "Usimwage chini nafsi yangu."

Maskili.* Wa Daudi,
alipokuwa pangoni.^a Sala.

142

Kwa sauti yangu
ninamlilia Yehova
anisaidie;^b

Kwa sauti yangu ninamsihi
Yehova anionyeshe
kibali.

2 Ninamwaga mahangaiko
yangu mbele zake;

Mbele zake ninaeleza taa-
bu yangu^c

3 Roho yangu inapozimia
ndani yangu.*

Ndipo unapoitazama bara-
bara yangu.^d

Katika njia ninayotembea,
Wanaficha mtego wa kuni-
nasa.

4 Tazama upande wa mkono
wangu wa kulia uone^e

Kwamba hakuna yeyote
anayenijali.*

Sina mahali popote pa ku-
kimbilia;^f

Hakuna yeyote anayeniha-
ngaikia.

5 Ninakulilia unisaidie, Ee
Yehova.

Ninasema: "Wewe ni ki-
mbilio langu,^g

Ni wewe tu niliye nawe*
katika nchi ya walio hai."

6 Sikiliza kilio changu cha
kuomba msaada,

Kwa maana nimeshushwa
chini sana.

Niokoe kutoka kwa wale
wanaonitesa,^h

Kwa maana wana nguvu
kuliko mimi.

7 Nitoe katika gereza lililo
chini ya ardhi

Ili nilisifu jina lako.

142:Uta *Angalia Kamusi, uku. 2012.
142:3 *Au "Ninapoishiwa na nguvu."
142:4 *Tnn., "anayenitambua." 142:5
*Tnn., "Fungu langu."

SURA YA 142

a 1Sa 22:1
1Sa 24:3
Ebr 11:32, 38

b Zb 28:2
Zb 141:1

c Zb 18:6
Yon 2:7
Mt 26:38, 39
Mk 15:34
Ebr 5:7

d Zb 139:3

e Zb 31:11
Zb 69:20

f 1Sa 23:11

g Met 18:10

h 1Sa 20:33
1Sa 23:26
1Sa 25:29

Safu ya 2

SURA YA 143

a Zb 65:2

b Ayu 9:2
Zb 130:3
Mhu 7:20
Ro 3:20
Gal 2:16
1Yo 1:10

c Zb 142:3

d Zb 102:4

e Zb 77:5, 6
Zb 77:11, 12
Zb 111:2, 3

f Zb 63:1

g Zb 40:13
Zb 70:5

h Zb 142:3

i Zb 27:9

Waadilifu na wakusanyike
kunizunguka

Kwa sababu unanitendea
kwa fadhili.

Muziki wa Daudi.

143

Ee Yehova, isikie
sala yangu;^a

Sikiliza sihi yangu ya kuo-
mba msaada.

Nijibu katika uaminifu
wako na katika uadilifu
wako.

2 Usinihakumu mimi mtu-
mishi wako,

Kwa maana hakuna yeyote
aliye hai anayeweza
kuwa mwadilifu mbele
zako.^b

3 Kwa maana adui anani-
fuatia;

Ameuponda uhai wangu
ardhini.

Amenifanya nikae gizani
kama wale waliokufa
zamani za kale.

4 Roho yangu inazimia;*^c
Moyo wangu umekufa
ganzi.^d

5 Ninazikumbuka siku za
kale;

Ninatafakari utendaji
wako wote;^e

Ninatafakari* kwa bidii
kazi ya mikono yako.

6 Ninakunyooshea mikono
yangu;

Mimi ni kama nchi iliyo-
kauka yenye kiu kwa ajili
yako.^f (Sela)

7 Nijibu haraka, Ee Yehova;^g
Nguvu zangu zimefikia*
mwisho.^h

Usinifiche uso wako,ⁱ

143:4 *Au "Ninaishiwa na nguvu."
143:5 *Au "Ninajifunza." 143:7 *Tnn.,
"Roho yangu imefikia."

La sivyo nitakuwa kama wale wanaoshuka shimoni.*^a

8 Acha nisikie upendo wako mshikamanifu asubuhi, Kwa maana ninakutumaini wewe.

Nijulishe njia ninayopaswa kutembea ndani yake,^b Kwa maana ninakugeukia wewe.*

9 Niokoe kutoka kwa maa-
dui wangu, Ee Yehova.
Ninatafuta ulinzi wako.^c

10 Nifundishe kufanya mape-
nzi yako,^d

Kwa maana wewe ni Mu-
ngu wangu.
Roho yako ni nzuri;
Na iniongoze kwenye nchi
tambarare.*

11 Ee Yehova, nihifadhi hai
kwa ajili ya jina lako.
Katika uadilifu wako, nio-
koe kutoka katika
taabu.^e

12 Katika upendo wako mshi-
kamanifu, waangamize*
maadui wangu;^f
Waangamize wote wanao-
ninyanyasa,^g
Kwa maana mimi ni mtu-
mishi wako.^h

Wa Daudi.

144 Yehova, Mwamba
wangu, na asifiwe,
Anayeizoeza mikono
yangu kwa ajili ya vita,
Vidole vyangu kwa ajili ya
kupigana.ⁱ

2 Yeye ni upendo wangu
mshikamanifu na ngome
yangu,

143:7 *Au "kaburini." **143:8** *Au "Kwa maana ninakuinulia nafsi yangu."
143:10 *Au "katika nchi ya unyoofu."
143:12 *Tnn., "wanyamazishe."

SURA YA 143

a Zb 28:1

b Zb 5:8
Met 3:6

c Zb 59:1
Zb 61:3, 4
Zb 91:1

d Zb 25:4

e Zb 31:1

f 1Sa 25:29
1Sa 26:9, 10

g 1Sa 24:12

h Zb 89:20

SURA YA 144

i Kum 32:4

j 2Sa 22:35
Zb 18:2, 34

Safu ya 2

a 2Sa 22:2, 3

b Zb 18:47

c Zb 8:4
Ebr 2:6

d Zb 39:5

e 1Nya 29:15
Ayu 14:1, 2

f Zb 18:9

g Kut 19:18

h Ayu 36:32

i 2Sa 22:15

j 2Sa 22:17, 18
Zb 18:16, 17
Zb 54:3

k Zb 33:3
Zb 40:3
Zb 96:1
Isa 42:10
Ufu 5:9
Ufu 14:3

l 2Sa 5:19
Zb 18:50

Kimbilio langu salama* na mwokozi wangu,
Ngao yangu na Yule amba-
ye nimejificha ndani
yake,^a

Yule anayeyatiisha matai-
fa chini yangu.^b

3 Ee Yehova, mwanadamu ni
nini hata umtambue,
Mwana wa mtu anayeweza
kufa ni nini hata umka-
zie uangalifu?^c

4 Mwanadamu ni kama
pumzi tu;^d

Siku zake ni kama kivuli
kinachopita.^e

5 Ee Yehova, shusha* mbi-
ngu zako uteremke;^f
Iguse milima na uifanye
ifuke moshi.^g

6 Ifanye radi imweke na
kuwatawanya maadui;^h
Piga mishale yako uwavu-
ruge.ⁱ

7 Inyooshe mikono yako
kutoka juu;
Niokoe na kuninusuru ku-
toka katika maji mengi,
Kutoka katika mkono* wa
wageni.^j

8 Ambao kinywa chao kina-
sema uwongo
Na ambao wanainua juu
mkono wao wa kulia ili
kuapa kwa uwongo.*

9 Ee Mungu, nitakuambia
wimbo mpya.^k

Nitakuambia sifa* kwa
kinanda cha nyuzi kumi,

10 Wewe unayewapa wafalme
ushindi,*^l

144:2 *Au "Kilele changu salama."

144:5 *Au "kunja." **144:7** *Au "udhibiti." **144:8** *Tnn., "Na mkono wao wa kulia ni mkono wa kulia wa uwongo." **144:9** *Au "Nitakupigia muziki." **144:10** *Au "wokovu."

Wewe unayemwokoa mtumishi wako Daudi kutokana na upanga hatari.^a

- 11** Niokoe na kuninusuru kutoka katika mkono wa wageni, Ambao vinywa vyao husema uwongo Na ambao wanainua mkonono wao wa kulia ili kuapa kwa uwongo.

- 12** Ndipo wana wetu watakuwa kama mimea michanga inayokua haraka, Mabinti wetu kama nguzo za pembeni zilizocho-ngwa kwa ajili ya jumba la mfalme.

- 13** Maghala yetu yatafurika mazao ya kila aina; Makundi yetu ya kondoo yataongezeka kwa mael-fu, kwa makumi ya maelfu.

- 14** Ng'ombe wetu, wakiwa na mimba, hawatapatwa na jambo baya* wala mimba kuharibika, Hakutakuwa na kilio cha kuteseka katika viwanja vyetu vya mji.

- 15** Wenye furaha ni watu wenye hali hizo! Wenye furaha ni watu ambao Mungu wao ni Yehova!^b

Sifa ya Daudi.

Ⲛ [Aleph]

145 Nitakukweza, Ee Mungu wangu Mfalme.^c

Nitalisifu jina lako milele na milele.^d

144:14 *Au "hawatapasukiwa na mimba."

SURA YA 144

a 1Sa 17:45, 46
2Sa 21:15, 17

b Zb 33:12
Zb 37:9
Zb 37:37
Zb 146:5

SURA YA 145

c Isa 33:22
Ufu 11:17

d 1Nya 29:10

Safu ya 2

a Zb 119:164

b Zb 146:2

c Zb 150:2
Ro 1:20
Ufu 15:3

d Ayu 26:14
Zb 139:6
Ro 11:33

e Kut 12:26, 27

f Zb 8:1

g 1Fa 8:66
Zb 13:6
Zb 31:19
Isa 63:7
Yer 31:12

h Zb 51:14
Ufu 15:3

i 2Nya 30:9
Efe 2:4

j Kut 34:6
Ne 9:17

k Zb 25:8
Nah 1:7
Mt 5:44, 45
Mdo 14:17
Yak 1:17

Ⲛ [Beth]

- 2** Nitakusifu mchana kutwa;^a Nitalisifu jina lako milele na milele.^b

ⲗ [Gimel]

- 3** Yehova ni mkuu na anastahili kabisa kusifiwa;^c Ukuu wake hauchunguziki.^{*d}

ⲧ [Daleth]

- 4** Kizazi baada ya kizazi kitasifu kazi zako; Watasimulia matendo yako yenye nguvu.^e

ⲧ [He]

- 5** Watasema kuhusu fahari tukufu ya ukuu wako^f Nami nitatafakari kazi zako zinazostaajibisha.

ⲧ [Waw]

- 6** Watasema kuhusu matendo yako yana-yoogopesha,^{*} Nami nitautangaza ukuu wako.

ⲧ [Zayin]

- 7** Watabubujikwa na maneno wanapokumbuka wema wako mwingi,^g Nao watapaza sauti kwa shangwe kwa sababu ya uadilifu wako.^h

ⲧ [Heth]

- 8** Yehova ni mwenye huruma* na rehema,ⁱ Si mwepesi wa hasira, naye ana upendo mwingi mshikamanifu.^j

Ⲛ [Teth]

- 9** Yehova ni mwema kwa wote,^k Na rehema zake zinaonekana katika kazi zake zote.

145:3 *Au "hauwezi kueleweka." **145:6** *Au "nguvu zako." **145:8** *Au "neema."

^ˆ [Yod]

10 Kazi zako zote zitakutukuza, Ee Yehova,^a
Na washikamanifu wako watakusifu.^b

[⊃] [Kaph]

11 Watatangaza utukufu wa ufalme wako^c
Na kusema kuhusu nguvu zako,^d

[↳] [Lamed]

12 Ili kuwajulisha wanadamu matendo yako yenye nguvu^e
Na fahari yenye utukufu ya ufalme wako.^f

[⊃] [Mem]

13 Ufalme wako ni ufalme wa milele,
Na mamlaka yako hudumu katika vizazi vyote.^g

[⊃] [Samekh]

14 Yehova huwategemeza wote wanaoanguka^h
Na kuwainua juu wote walioinama chini.ⁱ

[⊃] [Ayin]

15 Macho yote yanakutazama yakiwa na tumaini;
Unawapa chakula chao katika majira yake.^j

[⊃] [Pe]

16 Unaufumbua mkono wako Na kutosheleza tamaa ya kila kitu kilicho hai.^k

[⊃] [Tsade]

17 Yehova ni mwadilifu kati-ka njia zake zote^l
Na mshikamanifu katika kila jambo analotenda.^m

[⊃] [Qoph]

18 Yehova yuko karibu na wote wanaomwitia,ⁿ
Wote wanaomwitia yeye katika ukweli.^{*o}

145:18 *Au "kwa unyoofu."

SURA YA 145

a Zb 19:1
b Zb 30:4
Ebr 13:15
c Lu 10:8, 9
d Kum 3:24
1Nya 29:11
Ufu 15:3
e Zb 98:1
f Zb 103:19
g Zb 146:10
1Ti 1:17
h Zb 37:23, 24
Zb 94:18
i Zb 146:8
j Mwa 1:30
Zb 136:25
k Zb 104:27, 28
Zb 107:9
Zb 132:14, 15
l Mwa 18:25
Kum 32:4
m Zb 18:25
Ufu 15:3, 4
n Zb 34:18
Yak 4:8
o Zb 17:1

Safu ya 2

a Zb 34:9
b Zb 37:39, 40
Zb 50:15
c Zb 31:23
Zb 97:10
d Met 2:22
e Zb 34:1
Zb 51:15
f Zb 117:1
Zb 150:6

SURA YA 146

g Ufu 19:6
h Zb 103:1
i Zb 62:9
Zb 118:8, 9
Isa 2:22
Yer 17:5
j Mwa 3:19
Zb 104:29
Mhu 3:20
Mhu 12:7
k Mhu 9:5, 10
Isa 38:18
l Zb 46:7
m Zb 71:5
Yer 17:7
n Mdo 4:24
Ufu 14:7
o Kum 7:9

[⊃] [Resh]

19 Hutosheleza tamaa ya wale wanaomwogopa;^a
Husikia kilio chao cha kuomba msaada, naye huwaokoa.^b

[⊃] [Shin]

20 Yehova huwalinda wale wote wanaompenda,^c
Lakini atawaangamiza waovu wote.^d

[⊃] [Taw]

21 Kinywa changu kitangaza sifa za Yehova;^e
Kila kitu kilicho hai na kilisifu* jina lake takatifu milele na milele.^f

146 Msifuni Yah!^{*g}
Nafsi yangu yote na isifu Yehova.^h

2 Nitamsifu Yehova maisha yangu yote.
Nitamwambia sifa* Mungu wangu maadamu ninai-shi.

3 Msiwatumaini wakuu*
Wala mwanadamu, ambaye hawezi kuleta wokovu.ⁱ

4 Roho* yake hutoka, naye hurudi ardhini;^j
Siku hiyohiyo mwawo yake hupotea.^k

5 Mwenye furaha ni yule ambaye Mungu wa Yakobo ni msaidizi wake,^l
Ambaye anamtumaini Yehova Mungu wake,^m

6 Muumba wa mbingu na dunia,
Wa bahari, na vyote vilivyomo,ⁿ
Yeye ambaye ni mwaminifu daima,^o

145:21 *Tnn., "Miili yote na isifu."
146:1 *Au "Haleluya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova. 146:2 *Au "Nitampigia muziki." 146:3 *Au "viongozi." 146:4 *Au "Pumzi."

- 7 Yeye anayetekeleza haki kwa ajili ya waliopunjwa, Yeye anayewapa chakula* wenye njaa.^a
Yehova anawaachilia huru wafungwa.^{#b}
- 8 Yehova anafungua macho ya vipofu;^c
Yehova anawainua juu wale walioinama chini;^d
Yehova anawapenda waa-dilifu.
- 9 Yehova anawalinda wa-kaaji wageni;
Humtegemeza yatima na mjane,^e
Lakini huivuruga mipango ya waovu.^{*f}
- 10 Yehova atakuwa Mfalme milele,^g
Mungu wako, Ee Sayuni, kizazi baada ya kizazi.
Msifuni Yah!*

147 Msifuni Yah!*
Ni vema kumwambia sifa# Mungu wetu;

- Jinsi inavyopendeza na jinsi inavyofaa sana kumsifu yeye!^h
- 2 Yehova analijenga Yerusalemu;ⁱ
Huwakusanya pamoja watu wa Israeli waliota-wanywa.^j
- 3 Huwaponya waliovunjika moyo;
Huyafunga majeraha yao.
- 4 Huhesabu idadi ya nyota; Zote anaziita kwa majina.^k
- 5 Bwana wetu ni mkuu naye ana nguvu nyingi;^l
Uelewaji wake haupimiki.^m

146:7 *Tnn., "mkate." #Tnn., "waliofungwa." 146:9 *Au "huiipotosha njia ya waovu." 146:10; 147:1 *Au "Halelu-ya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova. 147:1 #Au "kumpigia muziki."

SURA YA 146

a Zb 107:9
Zb 145:16

b Zb 107:14
Zb 142:7

c Isa 29:18
Isa 35:5

d Zb 145:14
2Ko 7:6

e Kum 10:18
Zb 68:5

f Zb 145:20

g Kut 15:18
Da 6:26
Ufu 11:15

SURA YA 147

h Zb 135:3

i Zb 102:16

j Kum 30:1-3
Eze 36:24

k Isa 40:26

l Nah 1:3

m Isa 40:28
Ro 11:33

Safu ya 2

a Zb 37:11

b 1Fa 18:45
Yer 14:22
Mt 5:45

c Ayu 38:25-27
Isa 30:23

d Zb 136:25

e Ayu 38:41
Lu 12:24

f Isa 31:1
Ho 1:7

g 1Sa 16:7

h Mal 3:16

i Zb 33:18

j Law 26:6
Isa 60:17

k Kum 8:7, 8
Zb 132:14, 15

l Ayu 37:6

- 6 Yehova huwainua wapole,^a
Lakini huwatupa chini waovu.
- 7 Mwimbieni Yehova kwa shukrani;
Mwimbieni sifa Mungu wetu kwa kinubi,
- 8 Yeye anayezifunika mbingu kwa mawingu,
Yeye anayeiletea dunia mvua,^b
Yeye anayechipusha majani^c milimani.
- 9 Anawapa wanyama chakula,^d
Kunguru wachanga wanaokililia.^e
- 10 Hapendezwi na nguvu za farasi;^f
Wala havutiwi na miguu yenye nguvu ya mwana-mume.^g
- 11 Yehova anafurahishwa na wale wanaomwogopa,^h
Wale wanaongojea upendo wake mshikamanifu.ⁱ
- 12 Mtukuze Yehova, Ee Yerusalemu.
Msifu Mungu wako, Ee Sayuni.
- 13 Huyafanya makomeo ya malango ya jiji lako yawe imara;
Huwabariki wana wako walio ndani yako.
- 14 Huleta amani katika eneo lako;^j
Hukushibisha kwa ngano bora kabisa.^{*k}
- 15 Huituma amri yake duniani;
Neno lake hukimbia upesi sana.
- 16 Hutoa theluji kama safu;^l
Hutawanya theluji

147:14 *Tnn., "mafuta ya ngano."

nyembamba kama majivu tu.^a

- 17 Huyatupa chini mawe yake ya mvua* kama chembe za mkate.^b

Ni nani anayeweza kusta-himili baridi yake?^c

- 18 Hulituma neno lake, nayo inayeyuka.

Huufanya upepo wake uvume,^d maji yanatiririka.

- 19 Anamtangazia Yakobo neno lake,

Na Israeli masharti yake na hukumu zake.^e

- 20 Hajalifanyia hivyo taifa lingine lolote;^f

Hawajui lolote kuhusu hukumu zake.

Msifuni Yah!^{*g}

- 148** Msifuni Yah!<sup>*
Msifuni Yehova
kutoka mbinguni,^h</sup>

Msifuni katika vilele.

- 2 Msifuni, enyi malaika wake wote.ⁱ

Msifuni, enyi jeshi lake lote.^j

- 3 Msifuni, enyi jua na mwezi.

Msifuni, enyi nyota zote zinazong'aa.^k

- 4 Msifuni, enyi mbingu zilizozoo juu kabisa*^{*}

Na maji yaliyo juu ya mbingu.

- 5 Na vilisifu jina la Yehova, Kwa maana aliamuru, navyo vikaumbwa.^l

- 6 Huvifanya viendeleo kuwa imara milele na milele;^m Ametoa agizo ambalo halitapitilia mbali.ⁿ

147:17 *Au "Huitupa chini barafu yake." 147:20; 148:1, 14; 149:1 *Au "Halelu-ya!" "Yah" ni ufupisho wa jina Yehova. 148:4 *Tnn., "mbingu za mbingu."

SURA YA 147

a Ayu 38:29

b Yos 10:11

c Ayu 37:10

d Zb 148:8

e Kum 4:5

f Kut 19:5
Kut 31:16, 17
Kum 4:8
1Nya 17:21
Ro 3:1, 2

g Ufu 19:6

SURA YA 148

h Zb 89:5

i Zb 103:20
Lu 2:13

j Yer 32:18
Yud 14

k Zb 19:1

l Zb 33:6

m Zb 89:37

n Zb 119:91
Yer 31:35, 36
Yer 33:25

Safu ya 2

a Kut 9:23
Zb 107:25
Isa 30:30

b Zb 98:8

c 1Nya 16:33
Isa 44:23

d Isa 43:20

e Zb 2:10, 11

f Zb 8:1
Isa 12:4

g 1Fa 8:27
1Nya 29:11

SURA YA 149

h Zb 33:3
Zb 96:1
Isa 42:10
Ufu 5:9

i Zb 22:22

- 7 Msifuni Yehova kutoka duniani, Enyi viumbe wakubwa wa baharini na pia vilindi vyote vya maji,

- 8 Enyi radi na mvua ya mawe, theluji na mawingu mazito,

Ewe kimbunga, unayetekeleza neno lake,^a

- 9 Enyi milima na vilima vyote.^b

Enyi miti ya matunda na mierezi yote,^c

- 10 Enyi wanyama wa mwituni^d na wanyama wote wa kufugwa, Enyi viumbe mnaotambaa na ndege wenye mabawa,

- 11 Enyi wafalme wa dunia, nanyi mataifa yote, Enyi wakuu na waamuzi wote wa dunia,^e

- 12 Enyi vijana wa kiume na wa kike,^{*} Wazee pamoja na watoto.[#]

- 13 Na walisifu jina la Yehova, Kwa maana jina lake peke yake liko juu sana lisiweze kufikiwa.^f

Ukuu wake uko juu ya dunia na mbingu.^g

- 14 Ataikweza nguvu[#] ya watu wake, Kwa sifa ya washikamanifu wake wote, Ya wana wa Israeli, watu walio karibu naye.

Msifuni Yah!^{*}

- 149** Msifuni Yah!<sup>*
Mwimbieni Yehova
wimbo mpya;^h</sup>

Msifuni katika kutaniko la washikamanifu.ⁱ

148:12 *Tnn., "mabikira." #Au "Wakubwa kwa wadogo." 148:14 #Tnn., "pembe."

- 2** Watu wa Israeli na washangilie kwa sababu ya Muumba wao Mkuu;^a
Wana wa Sayuni na washangilie kwa sababu ya Mfalme wao.
- 3** Na walisifu jina lake kwa kucheza dansi^b
Na wamwimbie sifa* kwa tari na kinubi.^c
- 4** Kwa maana Yehova anawafurahia watu wake.^d
Anawapamba wapole kwa wokovu.^e
- 5** Washikamanifu na washangilie kwa utukufu;
Na wapaze sauti kwa shangwe vitandani mwao.^f
- 6** Nyimbo zinazomsifu Mungu na ziwe kooni mwao,
Na upanga wenye makali pande mbili uwe mkononi mwao,
- 7** Ili kuyalipiza kisasi mataifa
Na kuyaadhibu mataifa,
- 8** Ili kuwafunga wafalme wao kwa pingu
Na viongozi wao kwa pingu za chuma,
- 9** Ili kutekeleza hukumu iliyoandikwa kuwahusu.^g

149:3 *Au “wampigie muziki.”

SURA YA 149

a Zb 100:3

Isa 54:5

b Amu 11:34

c Kut 15:20

Zb 150:4

d Zb 84:11

e Zb 132:16

Isa 61:10

f Zb 63:6

g Kum 7:1

Safu ya 2

SURA YA 150

a Ufu 19:6

b Zb 116:19

c Zb 19:1

d Zb 107:15

Ufu 15:3

e Kum 3:24

Zb 145:3

f Zb 81:3

g 1Nya 15:28

h Kut 15:20

i Zb 92:1, 3

Zb 144:9

j 1Sa 10:5

k 2Sa 6:5

1Nya 15:19

1Nya 16:5

l Ufu 5:13

Heshima hii ni ya washikamanifu wake wote.

Msfuni Yah!*

150 Msfuni Yah! *^a
Msfuni Mungu katika mahali pake patakatifu.^b

Msfuni katika anga la*
nguvu zake.^c

2 Msfuni kwa kazi zake
zenye nguvu.^d

Msfuni kwa ukuu wake
usio na kifani.^e

3 Msfuni kwa kupiga pembe.^f

Msfuni kwa kinanda na kinubi.^g

4 Msfuni kwa tari^h na kwa dansi ya mzunguko.

Msfuni kwa nyuziⁱ na filimbi.^{*j}

5 Msfuni kwa matoazi yanayolia.

Msfuni kwa matoazi yanayogonganishwa.^k

6 Kila kitu kinachopumua
—na kimsifu Yah.

Msfuni Yah! *^l

149:9; 150:1, 6 *Au “Haleluya!” “Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. 150:1 *Au “anga linalotoa ushahidi kuhusu.” 150:4 *Au “zumari.”

METHALI

YALIYOMO

- 1** Kusudi la methali (1-7)
Hatari za marafiki wabaya (8-19)
Hekima ya kweli hupaza sauti hadharani (20-33)
- 2** Thamani ya hekima (1-22)
Tafuta hekima kama hazina zilizofichika (4)

- Uwezo wa kufikiri ni ulinzi (11)
Uasherati huleta msiba (16-19)
- 3** Uwe na hekima na umtumaini Yehova (1-12)
Mheshimu Yehova kwa vitu vyenye thamani (9)

- Hekima huleta furaha (13-18)
 Hekima huleta usalama (19-26)
 Mambo mema ya kuwatendea wengine (27-35)
 Watendee wengine mema inapowezekana (27)
- 4 Mafundisho ya baba yenye hekima (1-27)
 Zaidi ya yote, pata hekima (7)
 Epuka vijia vya uovu (14, 15)
 Kijia cha waadilifu huzidi kung'aa (18)
 "Ulinde moyo wako" (23)
- 5 Onyo dhidi ya wanawake waasherati (1-14)
 Shangilia pamoja na mke wako (15-23)
- 6 Jihadhari kuhusiana na kutoa dhamana ya mkopo (1-5)
 "Mwendee chungu, ewe mvivu" (6-11)
 Mtu mwovu asiyejaa kitu (12-15)
 Vitu saba ambavyo Yehova anachukia (16-19)
 Jilinde dhidi ya mwanamke mwovu (20-35)
- 7 Zishike amri za Mungu uishi (1-5)
 Kijana mjinga atongozwa (6-27)
 "Kama ng'ombe dume anayeenda machinjioni" (22)
- 8 Hekima yaongea kama mtu (1-36)
 'Mimi ni mwanzo kabisa wa kazi za Mungu' (22)
 'Nilikuwa kando ya Mungu nikiwa mfanyakazi stadi' (30)
 "Niliwapenda sana wanadamu" (31)
- 9 Hekima ya kweli inatoa mwaliko (1-12)
 "Nitafanya siku zako ziwe nyingi" (11)
 Mwanamke mpumbavu awaalika watu (13-18)
 "Maji yaliyoibwa ni matamu" (17)
- 10 METHALI ZA SULEMANI (10:1-24:34)
 Mwana mwenye hekima humfanya baba yake ashangilie (1)
 Mikono yenye bidii huleta utajiri (4)
 Kusema maneno mengi husababisha makosa (19)
 Baraka ya Yehova hutajirisha (22)
 Kumwogopa Yehova hurefusha maisha (27)
- 11 Wenye kiasi wana hekima (2)
 Mwasi imani huwaangamiza wengine (9)
 "Washauri wengi huleta mafanikio" (14)
- Mtu mkarimu atapata ufanisi (25)
 Anayeutumaini utajiri wake ataanguka (28)
- 12 Anayechukia karipio hana akili (1)
 "Maneno yanayosemwa bila kufikiri huchoma kama upanga" (18)
 Kusitawisha amani huleta shangwe (20)
 Midomo inayosema uwongo humchukiza Yehova (22)
 Mahangaiko huulemea moyo (25)
- 13 Wanaotafuta ushauri wana hekima (10)
 Tumaini likikawia huufanya moyo uwe mgonjwa (12)
 Mjumbe mwaminifu huleta maponyo (17)
 Kutembea na wenye hekima humfanya mtu awe na hekima (20)
 Nidhamu huonyesha upendo (24)
- 14 Moyo hujua uchungu wake wenyewe (10)
 Njia inayoonekana kuwa sawa inaweza kusababisha kifo (12)
 Mjinga huamini kila neno (15)
 Tajiri ana marafiki wengi (20)
 Moyo mtulivu huupa mwili uzima (30)
- 15 Jibu la upole hutuliza hasira (1)
 Macho ya Yehova yako kila mahali (3)
 Sala ya mtu mnyoofu humfurahisha Mungu (8)
 Mipango huvunjika watu wasiposhauriana (22)
 Tafakari kabla ya kujibu (28)
- 16 Yehova huchunguza nia (2)
 Mkabidhi Yehova kazi zako (3)
 Mizani ya unyoofu hutoka kwa Yehova (11)
 Kiburi hutangulia kuanguka kwa kishindo (18)
 Mvi ni taji la umaridadi (31)
- 17 Usilipe uovu kwa wema (13)
 Ondoka kabla ugomvi haujaanza (14)
 Rafiki wa kweli hupenda nyakati zote (17)
 "Moyo wenye shangwe ni dawa nzuri" (22)
 Mtu mwenye utambuzi huyazuia maneno yake (27)
- 18 Kujitenga na wengine ni jambo la kichoyo lisilo la hekima (1)
 Jina la Yehova ni mnara wenye nguvu (10)

- Mali ni ulinzi wa kuwaziwa tu (11)
 Hekima ya kusikiliza pande zote mbili (17)
 Rafiki hushikamana na mtu kwa ukaribu kuliko ndugu (24)
- 19 Ufafanuzi hutuliza hasira (11)
 Mke mgomvi ni kama paa linalovuja (13)
 Mke mwenye busara hutoka kwa Yehova (14)
 Mtie mtoto nidhamu wakati bado kuna tumaini (18)
 Hekima ya kusikiliza mashauri (20)
- 20 Divai ni mdhahiki (1)
 Mvivu halimi katika majira ya baridi kali (4)
 Mawazo ya mtu ni kama maji yenye kina (5)
 Onyo dhidi ya kuapa haraka-haraka (25)
 Utukufu wa vijana ni nguvu zao (29)
- 21 Yehova huelekeza moyo wa mfalme (1)
 Haki ni bora kuliko dhahiki (3)
 Bidii huleta mafanikio (5)
 Asiyemsikiliza mtu wa hali ya chini hata sikilizwa (13)
 Hakuna hekima katika kumpinga Yehova (30)
- 22 Jina jema ni bora kuliko mali nyingi (1)
 Mazoezi ya mapema ya mtoto yataidumu maisha yake yote (6)
 Mvivu huogopa kwamba simba yuko nje (13)
 Nidhamu huondoa ujinga (15)
 Mfanyakazi stadi huwatumikia wafalme (29)
- 23 Uwe na busara unapokubali mwaliko (2)
 Usifuatie utajiri (4)
 Utajiri unaweza kuruka mbali nawe (5)
 Usiwe miongoni mwa walevi (20)
 Kileo huuma kama nyoka (32)
- 24 Usiwaonee wivu waovu (1)
 Nyumba hujengwa kwa hekima (3)
 Mwadilifu anaweza kuanguka lakini atainuka (16)
 Usilipize kisasi (29)
 Kusinzia huleta umaskini (33, 34)
- 25 METHALI ZA SULEMANI ZILIZONAKILIWA NA WATU WA MFALME HEZEKIA (25:1-29:27)
 Kutunza siri (9)
 Maneno yaliyochaguliwa vizuri (11)
- Kuheshimu faragha ya wengine (17)
 Kukusanya makaa ya mawe juu ya kichwa cha adui (21, 22)
 Habari njema ni kama maji baridi (25)
- 26 Ufafanuzi kuwahusu watu wavivu (13-16)
 Epuka ugomvi usiokuhusu (17)
 Epuka mizaha inayodhuru (18, 19)
 Pasipo na kuni, moto huzimika (20, 21)
 Maneno ya mchongezi ni kama matonge matamu (22)
- 27 Karipio kutoka kwa rafiki hunufaisha (5, 6)
 Mwanangu, ufanye moyo wangu ushangilie (11)
 Chuma hunoa chuma (17)
 Lijue kundi lako (23)
 Mali haidumu milele (24)
- 28 Sala ya mtu asiyesikiliza inachukiza (9)
 Anayeungama huonyeshwa rehemu (13)
 Anayeharakisha kupata utajiri hatakosha hatia (20)
 Karipio ni bora kuliko kusifusifu (23)
 Mtu mkarimu hakosi chochote (27)
- 29 Mtoto aliyechuliwa huleta aibu (15)
 Bila maono, watu hutenda wapendavyo (18)
 Mtu mwenye hasira huchochea ugomvi (22)
 Mtu mnyenyekevu hupata utukufu (23)
 Kuwaogopa wanadamu ni mtego (25)
- 30 MANENO YA AGURI (1-33)
 Usinipe umaskini wala utajiri (8)
 Vitu visivyotosheka kamwe (15, 16)
 Vitu visivyoacha alama (18, 19)
 Mwanamke mzinzi (20)
 Wanyama wenye hekima ya kisilika (24)
- 31 MANENO YA MFALME LEMUELI (1-31)
 Ni nani anayeweza kumpata mke mwema? (10)
 Hufanya kazi kwa bidii na jitihada (17)
 Fadhili ziko kwenye ulimi wake (26)
 Watoto wake na mume wake hufusifu (28)
 Sura nzuri na urembo hutoweka upesi (30)

1 Methali za Sulemani^a mwana wa Daudi,^b mfalme wa Israeli:^c

- 2** Ili mtu ajifunze* hekima^d na nidhamu;
Ili aelewe maneno ya hekima;
- 3** Ili apate nidhamu^e inayoleta ufahamu,
Uadilifu,^f busara,^{*g} na unyoofu;[#]
- 4** Ili kumfanya mjinga awe mwerevu;^h
Ili kumpa kijana ujuzi na uwezo wa kufikiri.ⁱ
- 5** Mtu mwenye hekima husikiliza na kujifunza zaidi;^j
Mtu mwenye uelewaji hupata mwelekezo stadi*^k
- 6** Ili kuelewa methali na fumbo,*
Maneno ya wenye hekima na vitendawili vyao.^l
- 7** Kumwogopa* Yehova ndio mwanzo wa ujuzi.^m
Ni wapumbavu tu wanaodharau hekima na nidhamu.ⁿ
- 8** Mwanangu, sikiliza nidhamu ya baba yako,^o
Wala usiyaache mafundisho* ya mama yako.^p
- 9** Ni shada linalovutia kwenye kichwa chako^q
Na pambo maridadi shingoni mwako.^r
- 10** Mwanangu, watenda dhambi wakijaribu kukushawishi, usikubali.^s
- 11** Wakisema: "Njoo twende. Acha tuvizie ili kumwaga damu.
Tutajificha na kuwasha-

1:2 *Au "ajue." 1:3 *Au "jambo lili la haki." #Au "kutokuwa na ubaguzi." 1:5 *Au "mwongozo wenye hekima." 1:6 *Au "mfano." 1:7 *Au "Kumheshimu." 1:8 *Au "usiiache sheria."

SURA YA 1

a 1Fa 4:29, 32
Mhu 12:9

b 2Sa 12:24

c 1Fa 2:12

d Met 8:11

e Met 3:11, 12

f Ebr 12:11

g 1Fa 3:28

h Met 15:5

i Met 2:11

Met 3:21
Met 8:12

j Met 9:9

k 1Sa 25:32, 33
Met 24:6

l Mhu 12:11

m Ayu 28:28
Met 9:10

n Met 5:12, 13
Met 18:2

o Kum 6:6, 7
Efe 6:4
Ebr 12:9

p Law 19:3
Met 31:26
2Ti 1:5

q Met 4:7, 9

r Met 3:21, 22

s Mwa 39:7, 8
Kum 13:6-8

Safu ya 2

a Met 4:14
Met 13:20
1Ko 15:33

b Met 6:16-18
Ro 3:15

c Met 15:27

d Ro 16:27
1Ko 1:20
Yak 3:17

e Mt 10:27

f Met 8:1-3
Met 9:1, 3

mbulia bila sababu watu wasio na hatia.

- 12** Tutawameza wakiwa hai kama Kaburi* linavyomeza,
Wazima-wazima, kama wale wanaoshuka shimoni.
- 13** Na tunyakue mali zao zote zenye thamani;
Nyumba zetu tutazijaza nyara.
- 14** Unapaswa kujiunga nasi,*
Nasi sote tutagawana sawasawa vitu tuna-
vyoiba."#
- 15** Mwanangu, usiwafuate.
Iepushe miguu yako na njia yao.^a
- 16** Kwa maana miguu yao hukimbilia kutenda uovu;
Wanaenda haraka kumwaga damu.^b
- 17** Kwa kweli ni kazi bure kutandaza wavu huku ndege akitazama.
- 18** Ndio sababu wanavizia ili kumwaga damu;
Wanajificha ili wawaue* wengine.
- 19** Hizo ndizo njia za wale wanaotafuta faida isiyo ya haki,
Ambayo itawaangamiza wale wanaoipata.^c
- 20** Hekima ya kweli^d hupaza sauti kubwa barabarani.^e
Huendelea kuinua sauti yake katika viwanja vya jiji.^f
- 21** Hupaza sauti kwenye makutano ya barabara zenye watu wengi.

1:12 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 1:14 *Au "Liweke fungu lako pamoja na letu." #Au "tutakuwa na mfuko mmoja (kibeti kimoja)." 1:18 *Au "waangamize nafsi za."

- Nayo husema hivi kwenye malango ya jiji:^a
- 22** “Ninyi wajinga mtaendelea kuupenda ujinga mpaka lini?
Nanyi wadhuhaki mtaendelea kufurahia dhuhaka mpaka lini?
Nanyi wapumbavu mtaendelea kuchukua ujuzi mpaka lini?^b
- 23** Sikilizeni karipio langu.^{*c}
Ndipo nitakapowamiminia roho yangu;
Nitawajulisha maneno yangu.^d
- 24** Kwa sababu niliwaita, lakini mkaendelea kukataa,
Niliunyoosha mkono wangu, lakini hakuna yeyote aliyejali,^e
- 25** Mliendelea kupuuza ushauri wangu wote
Na kukataa karipio langu,
- 26** Mimi pia nitawacheka mtakapopatwa na msiba;
Nitawadhuhaki jambo mnaoogopa litakapokuja,^f
- 27** Jambo mnaoogopa litakapokuja kama dhoruba,
Na msiba wenu utakapofika kama upepo wa dhoruba,
Wakati dhiki na taabu zitakapowapata.
- 28** Wakati huo wataendelea kuniita, lakini sitajibu;
Watanitafuta kwa bidii, lakini hawataniyata,^g
- 29** Kwa sababu walichukua ujuzi,^h
Nao hawakuchagua kumwogopa Yehova.ⁱ
- 30** Walikataa ushauri wangu; Waliyadharau makaripio yangu yote.

1:23 *Au “Geukeni ninapowakaripia.”

SURA YA 1

a Yoh 18:20
Mdo 20:20

b Met 5:12, 13
Yoh 3:20

c Zb 141:5
Ufu 3:19

d Isa 54:13

e Isa 65:12

f Amu 10:13, 14

g Omb 3:44

h Ho 4:6

i Amu 5:8

Safu ya 2

a Yer 6:19
Gal 6:7

b Isa 48:18

c 2Fa 6:15, 16
Isa 26:3
2Pe 2:9

SURA YA 2

d Kum 6:6, 8

e Met 1:5

f Ebr 5:14

g 1Fa 3:11, 12
Met 9:10
ZTi 2:7

h Flp 1:9

i Zb 19:9, 10

j Ayu 28:15-18

k Ayu 28:28
Met 8:13
Yer 32:40

l Yer 9:24
1Yo 5:20

m Kut 31:2, 3
1Fa 4:29
ZTi 3:16, 17
Yak 3:17

n Zb 41:12
Met 28:18

o Zb 97:10

- 31** Basi watapata matokeo*
ya njia yao,^a
Nao watashiba kabisa ma-
shauri yao[#] wenyewe.

- 32** Kwa maana upotovu wa
wajinga utawaua,
Na kutojali kwa wapumba-
vu kutawaangamiza.

- 33** Lakini yule anayenisikili-
za ataishi kwa usalama^b
Naye hatahangaishwa na
woga wa msiba.^c

- 2** Mwanangu, ukiyakubali
maneno yangu
Na kuhifadhi amri zangu
kama hazina,^d

- 2** Kwa kutega sikio lako usi-
kilize hekima^e
Na kuuelekeza moyo wako
upate utambuzi;^f

- 3** Pia, ukiuita uelewaji kwa
sauti^g
Na kupaza sauti yako upa-
te utambuzi;^h

- 4** Ukiendelea kuutafuta
kama fedha,^{*i}
Na kuendelea kuutafuta
sana kama hazina zilizo-
fichika;^j

- 5** Ndipo utakapoelewa
kumwogopa Yehova,^k
Nawe utapata ujuzi
kumhusu Mungu.^l

- 6** Kwa maana Yehova mwe-
nyewe hutoa hekima;^m
Na kinywani mwake huto-
ka ujuzi na utambuzi.

- 7** Huwahifadhia wanyoofu
hekima inayotumika;
Yeye ni ngao kwa wanao-
tembea kwa utimilifu.ⁿ

- 8** Huvilinda vijija vya haki,
Naye atailinda njia ya
washikamanifu wake.^o

1:31 *Tnn., “watakula matunda.” #Au
“njama zao; mipango yao.” 2:4 *Yaani,
madini ya fedha.

- 9 Ndipo utakapoelewa lililo la uadilifu na la haki na lililo sawa, Njia yote ya lililo jema.^a
- 10 Hekima inapoingia moyoni mwako^b Na ujuzi kupendeza nafsi* yako,^c
- 11 Uwezo wa kufikiri utakuinga,^d Na utambuzi utakulinda,
- 12 Ili kukuokoa kutoka kwenye njia mbaya, Kutoka kwa mtu anayesema mambo mapotovu,^e
- 13 Kutoka kwa wale wanaoviacha vijia vya unyoofu Ili watembe katika njia za giza,^f
- 14 Kutoka kwa wale wanaoshangilia kutenda mabaya, Wanaofurahia upotovu wa uovu,
- 15 Wale ambao vijia vyao vimepinda Na ambao mwenendo wao wote ni wenye hila.
- 16 Utakuokoa kutoka kwa mwanamke aliye potoka,* Kutoka kwa maneno laini[#] ya mwanamke mwashe-rati,^{*g}
- 17 Anayemwacha rafiki wa karibu* wa ujana wake^h Na kusahau agano la Mungu wake;
- 18 Kwa maana nyumba yake huzama katika kifo, Na vijia vyake* huongoza kwa wale waliokufa ambao hawana uwezo.ⁱ

2:10 *Angalia Kamusi, uku. 2:16 *Tnn., "mgeni." Ni wazi kwamba ni mgeni machoni pa Mungu kwa sababu ya upotovu wa maadili. [#]Au "maneno yenye ushawishi." 2:17 *Au "mume." 2:18 *Tnn., "mapito yake."

SURA YA 2

a Mhu 12:13
Mik 6:8
Mt 22:37-40

b Zb 119:111

c Mdo 17:11

d Mhu 7:12

e Met 8:13

f Yoh 3:19

g Mwa 39:10-12
Met 6:23, 24
Met 7:4, 5

h Mwa 2:24
Met 5:18

i Met 5:3, 5
Met 5:20, 23
Met 9:16-18
Efe 5:5

Safu ya 2

a Mhu 7:26
Ufu 22:15

b Met 13:20

c Zb 37:11, 29

d Zb 104:35
Met 10:7
Mt 25:46

e Kum 28:45, 63

SURA YA 3

f Kum 5:16

g Ho 12:6

h Kum 6:6, 8

i 2Ko 8:21

j Isa 26:4
Yer 17:7

k Met 28:26
Yer 10:23
1Ko 3:18

l 1Sa 23:2, 4
Ne 1:11
Flp 4:6

m Yos 1:7
Zb 25:9
Yak 1:5

- 19 Hakuna yeyote anayelala naye* atakayerudi, Wala hawatarudi kwenye vijia vya uzima.^a
- 20 Basi fuata njia ya watu wema Na ubaki kwenye vijia vya waadilifu,^b
- 21 Kwa maana ni wanyoofu tu watakaokaa duniani, Na wasio na lawama* ndio watakaobaki ndani yake.^c
- 22 Lakini waovu, wataangamizwa kutoka duniani,^d Na wenye hila watang'olewa kutoka ndani yake.^e
- 3 Mwanangu, usisahau mafundisho* yangu, Na moyo wako ushike amri zangu,
- 2 Kwa sababu zitakuongeza siku nyingi Na miaka ya uhai na amani.^f
- 3 Usiruhusu upendo mshikamanifu na uaminifu* zikuache.^g Zifunge shingoni mwako; Ziandike kwenye kibao cha moyo wako;^h
- 4 Ndipo utakapopata kibali na ufahamu mzuri Machoni pa Mungu na wanadamu.ⁱ
- 5 Mtumaini Yehova/ kwa moyo wako wote, Wala usitegemee* uelewaji wako mwenyewe.^k
- 6 Katika njia zako zote mtambue yeye,^l Naye atavinyoosha vijia vyako.^m

2:19 *Tnn., "anayeingia kwake." 2:21 *Au "wanaoshika utimilifu." 3:1 *Au "sheria." 3:3 *Au "ukweli." 3:5 *Tnn., "usitegemee."

- 7** Usiwe mwenye hekima machoni pako mwenyewe.^a
Mwogope Yehova na ujiepushe na uovu.
- 8** Hilo litaponya mwili wako*
Na kuiburudisha mifupa yako.
- 9** Mheshimu Yehova kwa vitu vyako vyenye thamani,^b
Kwa mavuno ya kwanza ya* mazao[#] yako yote;^c
- 10** Ndipo maghala yako yatakapojazwa kabisa,^d
Na mitungi yako itafurika* divai mpya.
- 11** Mwanangu, usikatae ndhamu ya Yehova,^e
Wala usichukie karipio lake,^f
- 12** Kwa maana Yehova huwakaripia wale anaowapenda,^g
Kama baba anavyomkaripia mwana anayempenda.^h
- 13** Mwenye furaha ni mtu anayepata hekimaⁱ
Na mtu anayepata utambuzi;
- 14** Kupata hekima ni bora kuliko kupata fedha,
Na kuipata kama faida ni bora kuliko kupata dhahabu.^j
- 15** Ni yenye thamani kuliko marijani*
Hakuna chochote unachotamani kinachoweza kulinganishwa nayo.

3:8 *Tnn., "kitovu chako." 3:9 *Au "vitu vilivyo bora vya." [#]Au "mapato." 3:10 *Au "mashinikizo yako ya divai yatafurika." 3:15 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 3

a Met 26:12
Ro 12:16

b Hes 31:50
Kum 16:16
Lu 16:9
ITI 6:18

c Kut 23:19

d 2Nya 31:10
Mal 3:10

e Met 15:32
Ebr 12:5, 6

f Zb 94:12

g Ufu 3:19

h Kum 8:5
Ebr 12:7, 9

i Mhu 7:12

j Ayu 28:15, 18

Safu ya 2

a Flp 4:9

b Zb 1:1, 2

c Zb 104:24

d Met 8:27
Yer 10:12

e Ayu 36:27
Ayu 38:37
Yer 10:13

f Isa 26:7

g Zb 3:5
Met 6:22

h Mhu 5:12

i Zb 27:1

j Zb 73:12, 19

k Met 10:29
Met 28:1

- 16** Maisha marefu yako katika mkono wake wa kulia;
Na katika mkono wake wa kushoto kuna utajiri na utukufu.
- 17** Njia zake zinapendeza,
Na vijia vyake vyote vina amani.^a
- 18** Ni mti wa uzima kwa wale wanaoishika,
Na wale wanaoishika kwa nguvu wataitwa wenye furaha.^b
- 19** Yehova aliuweka msingi wa dunia kwa hekima.^c
Aliziimarisha kabisa mbingu kwa utambuzi.^d
- 20** Kwa ujuzi wake vilindi vya maji vilitenganishwa
Na anga zenye mawingu zilidondosha umande.^e
- 21** Mwanangu, zisiondoke machoni pako.*
Ilinde hekima inayotumika na uwezo wa kufikiri;
- 22** Zitakupa uzima
Na kuwa pambo shingoni mwako;
- 23** Ndipo utakapotembea kwa usalama katika njia yako,
Na mguu wako hautaji kwaa kamwe.^{*f}
- 24** Unapolala, hutaogopa;^g
Utalala, na usingizi wako utakuwa mtamu.^h
- 25** Hutaogopa tisho lolote la ghafilaⁱ
Wala dhoruba inayowajia waovu.^j
- 26** Kwa maana Yehova atathibitika kuwa chanzo cha uhakika wako;^k

3:21 *Ni wazi kwamba mstari huu unarejelea sifa za Mungu zinazotajwa katika mistari iliyotangulia. 3:23 *Au "hautaogopa kamwe kitu chochote."

- Ataulinda mguu wako usinaswe.^a
- 27 Usiwanyime mema wale unaopaswa kuwatendea mema^{*b}
Ikiwa una uwezo wa kuwasaidia.^{*c}
- 28 Usimwambie jirani yako, “Nenda; rudi baadaye! Nitakupa kesho,”
Ikiwa unaweza kumpa kitu hicho sasa.
- 29 Usipange kumdhuru jirani yako^d
Anayejihisi akiwa salama mkiwa pamoja.
- 30 Usigombane na mtu bila sababu^e
Ikiwa hajakutendea jambo lolote baya.^f
- 31 Usimwonee wivu mtu mkatili^g
Wala kuchagua yoyote kati ya njia zake,
- 32 Kwa maana Yehova humchukia mtu mwenye hila,^h
Lakini ana urafiki wa karibu na watu wanyoofu.ⁱ
- 33 Laana ya Yehova iko juu ya nyumba ya mwovu,^j
Lakini huyabariki makao ya mwadilifu.^k
- 34 Kwa maana yeye huwadhihakia wale wanaodhihaki,^l
Lakini huwaonyesha kibali wapole.^m
- 35 Wenye hekima watarithi heshima,
Lakini wapumbavu hutukuza aibu.ⁿ
- 4** Wanangu, sikilizeni nidhamu ya baba;^o
Sikilizeni kwa makini ili mpate uelewaji,

3:27 *Au “wale wanaostahili.” # Au “Ikiwa mkono wako una nguvu za kusaidia.”

SURA YA 3

- a Zb 91:14
b Yak 2:15, 16
c Kum 15:7, 8
Met 28:27
d Met 6:16, 18
e Met 18:6
Met 20:3
f Ro 12:18
g Zb 37:1
Met 23:17
h Met 6:16, 17
i Zb 15:1, 2
Zb 24:3, 4
Zb 25:14
j Kum 28:15
Yos 7:24, 25
Est 9:24, 25
k Ayu 42:12, 13
Zb 37:25
l Met 19:29
m Zb 37:11
Zb 138:6
Isa 57:15
Yak 4:6
n Est 6:11, 12
Met 12:8

SURA YA 4

- o Kum 6:6, 7
Met 19:20
Efe 6:1
- Safu ya 2
a 1Nya 28:9
b 1Fa 2:12
c 1Fa 1:16-21
d Kum 4:9
e Law 18:5
f Ne 8:3, 8
Met 9:10
g Mhu 7:12
h Met 15:14
Mt 13:23
Ebr 5:14
i Da 1:17, 20
j 1Fa 4:29
k Kum 5:16
l 1Fa 4:29
m Isa 26:7
n Met 8:10
Ebr 2:1
Ebr 12:5, 6

- 2 Kwa maana nitawapa mafundisho mema; Msiache mafundisho* yangu.^a
- 3 Nilikuwa mwana halisi wa baba yangu^b
Na mama yangu alinipe-nda sana.^c
- 4 Baba alinifundisha na kusema: “Moyo wako na ushike kabisa maneno yangu.^d
Shika amri zangu, uendelee kuishi.^e
- 5 Jipatie hekima, jipatie uelewaji.^f
Usisahau, wala usiache ninayosema.
- 6 Usiiache, nayo itakukinga. Ipende, nayo itakulinda.
- 7 Hekima ndilo jambo muhimu zaidi,^{*g} kwa hiyo jipatie hekima, Pamoja na vyote unavyojipatie, jipatie uelewaji.^h
- 8 Ithamini sana, nayo itakukweza.ⁱ
Itakuheshimu kwa sababu unaikumbatia.^j
- 9 Itakuvika shada lenye kuvutia kichwani; Itakupamba kwa taji maredadi.”
- 10 Mwanangu, sikiliza maneno yangu na uyakubali, Na miaka ya maisha yako itakuwa mingi.^k
- 11 Nitakufundisha katika njia ya hekima;^l
Nitakuongoza katika vijia vya unyoofu.^m
- 12 Unapotembea, hatua zako hazitazuiwa; Na ukikimbia, hutajikwaa.
- 13 Shika kabisa nidhamu; usiache.ⁿ
- 4:2 *Au “sheria.” 4:7 *Au “la msingi.”

- Ilinde, kwa maana ni uzi-
ma wako.^a
- 14** Usiingie katika kijia cha
waovu,
Wala usitembee katika njia
ya watu wabaya.^b
- 15** Iepuke, usiifuute;^c
Jiepushe nayo, pita mbali
nayo.^d
- 16** Kwa maana hawawezi ku-
lala wasipotenda uovu.
Hawapati usingizi wasipo-
mwangusha mtu.
- 17** Wanajilisha mkate wa
uovu,
Na kunywa divai ya ukatili.
- 18** Lakini kijia cha waadilifu
ni kama nuru nyangavu
ya asubuhi
Inayong'aa zaidi na zaidi
mpaka mchana kamili.^e
- 19** Njia ya waovu ni kama
giza;
Hawajui ni nini kinacho-
wafajuni wajikwae.
- 20** Mwanangu, sikiliza mane-
no yangu;
Sikiliza kwa makini* nina-
yokwambia.
- 21** Yasiondoke machoni
pako;
Yaweke ndani kabisa mo-
yoni mwako,^f
- 22** Kwa maana ni uzima kwa
wale wanaoyapata^g
Na afya kwa mwili wao
wote.
- 23** Ulinde moyo wako kuliko
vitu vyote unavyolinda,^h
Kwa maana humo ndimo
zinamotoka chemchemi
za uzima.
- 24** Jiepushe kabisa na mane-
no yaliyopotoka,ⁱ
Na ujitenge mbali na ma-
zungumzo yenye hila.

4:20 *Tnn., "Yategee sikio."

SURA YA 4

a Kum 32:45-47
Ebr 12:11

b Zb 1:1
1Ko 15:33

c Amo 5:15
Efe 5:11

d Met 5:3, 8
1Th 5:22

e 2Sa 23:3, 4
Zb 119:105
1Ko 13:12
2Ko 4:6
2Pe 1:19

f Zb 40:8
Met 2:1

g 1Ti 4:8

h Yer 17:9
Mk 7:21-23
Efe 6:14

i 1Pe 2:1

Safu ya 2

a Mt 6:22

b Efe 5:15

c Kum 12:32
Yos 1:7

SURA YA 5

d 1Fa 4:29
Yak 1:19

e Met 15:7

f Met 7:14-21

g Met 9:16, 17

h Mhu 7:26

i Met 6:32, 33

25 Macho yako yanapaswa
kutazama mbele moja
kwa moja,

Naam, yakaze macho
yako* moja kwa moja
mbele yako.^a

26 Lainisha* mapito ya mi-
guu yako,^b

Na njia zako zote zitakuwa
thabiti.

27 Usielekee kulia wala
kushoto.^c

Iepushe miguu yako na
lililo ovu.

5 Mwanangu, sikiliza heki-
ma yangu.

Sikiliza kwa makini* uta-
mbuzi wangu,^d

2 Ili uweze kuulinda uwezo
wako wa kufikiri

Na kuulinda ujuzi kwa
midomo yako.^e

3 Kwa maana midomo ya
mwanamke aliyepotoka*
inadondoka kama sega la
asali,^f

Na kinywa chake ni laini
kuliko mafuta.^g

4 Lakini mwishowe ni
mchungu kama
pakanga^h

Na mwenye makali kama
upanga unaokata kwa
pande zote mbili.ⁱ

5 Miguu yake hushuka kwe-
nye kifo.

Hatua zake huongoza moja
kwa moja Kaburini.*

6 Hakazii fikira kijia cha
uzima.

Huyumbayumba katika
njia yake, lakini hajui
inakoeelekea.

4:25 *Au "macho yako yanayong'aa."

4:26 *Au labda, "Chunguza kwa ma-
kini." 5:1 *Tnn., "Utegee sikio." 5:3
*Tnn., "mgeni." Angalia Met 2:16. 5:5
*Au "Sheoli." Angalia Kamusi,
uku. 2012.

- 7** Sasa, wanangu, nisikilizeni
Nanyi msiache ninayo-sema.
- 8** Kaeni mbali naye;
Msiukaribie mlango wa nyumba yake,^a
- 9** Ili msiwape wengine heshima yenu^b
Wala kuvuna miaka ya ukatili;^c
- 10** Ili wageni wasimalize mali* zenu^d
Na vitu mlivyopata kwa jasho viende katika nyumba ya mgeni.
- 11** La sivyo, mtalia kwa uchungu mwishoni mwa maisha yenu
Nyama na mwili wenu vitakapodhoofika^e
- 12** Nanyi msemi: "Jinsi nilivyochukia nidhamu!
Jinsi moyo wangu ulivyo-dharau karipio!"
- 13** Sikusikiliza sauti ya waku-funzi wangu
Wala kuwasikiliza kwa makini walimu wangu.
- 14** Nimefika ukingoni mwa maangamizi kamili
Katikati ya kutaniko lote."^{*f}
- 15** Kunywa maji ya tangi lako mwenyewe
Na maji yanayotiririka* kutoka katika kisima chako mwenyewe.^g
- 16** Je, chemchemi zako zita-wanywe nje,
Na vijito vyako vya maji katika viwanja vya jiji?^h
- 17** Na yawe yako peke yako,
Wala si wageni pamoja nawe.ⁱ

5:10 *Au "nguvu." 5:14 *Tnn., "Katikati ya kusanyiko na kutaniko." 5:15 *Au "baridi."

SURA YA 5

a Met 9:14, 15

b Met 29:3

c Met 6:33-35
Met 7:23d Met 31:3
Lu 15:30

e Met 7:22, 23

f Met 6:27-29

g 1Ko 7:3
Ebr 13:4

h Met 5:20

i Mwa 2:24

Safu ya 2

a Kum 24:5
Mhu 9:9

b Wim 2:9

c Mwa 26:8
Mwa 29:20
Wim 8:6

d Met 22:14

e 2Nya 16:9
Zb 11:4
Zb 17:3
Yer 17:10
Ebr 4:13f Zb 7:14-16
Gal 6:7

SURA YA 6

g Met 17:18

h Met 11:15
Met 20:16

i Met 18:7

- 18** Chemchemi yako na ibarikiwe,*
Na ushangilie pamoja na mke wa ujana wako,^a
- 19** Paa jike anayependeza, mbuzi wa mlimani* anayevutia.^b
Matiti yake na yakuridhishe[#] nyakati zote.
Upendo wake na ukusisimue daima.^c
- 20** Basi mwanangu, kwa nini usisimuliwe na mwanamke aliyepotoka*
Au kukikumbatia kifua cha mwanamke mwashe-rati?*"d
- 21** Kwa maana njia za mwanadamu ziko mbele ya macho ya Yehova;
Yeye huvichunguza vijia vyake vyote.^e
- 22** Mwovu hunaswa na makosa yake mwenyewe,
Naye atashikwa na kamba za dhambi yake mwenyewe.^f
- 23** Atakufa kwa sababu ya utovu wa nidhamu
Na kupotea njia kwa sababu ya upumbavu wake uliopita kiasi.
- 6** Mwanangu, ikiwa ume-mdhamini* jirani yako,^g
Ikiwa umempa mkono[#] mtu usiyemjua,^h
- 2** Ikiwa umenaswa na ahadi yako,
Ukakamatwa na maneno ya kinywa chako,ⁱ
- 3** Mwanangu, fanya hivi ili ujiokoe,

5:18 *Au "Chanzo chako cha maji na kibarikiwe." 5:19 *Au "mbuzi mwitu." #Au "yakuleweshe." 5:20 *Tnn., "mgeni." Angalia Met 2:16. 6:1 *Tnn., "umemwekea dhama." #Yaani, Unapomdhamini.

- Kwa maana umeanguka mikononi mwa jirani yako:
Nenda ujinyenyekeze mwenyewe na kumsihi haraka jirani yako.^a
- 4** Usiruhusu macho yako yapatwe usingizi,
Wala kope zako kusinzia.
- 5** Jiokoe kama swala kutoka mikononi mwa mwindaji,
Kama ndege kutoka mikononi mwa mwindaji wa ndege.
- 6** Mwendee chungu, ewe mvivu,^b
Zichunguze njia zake uwe na hekima.
- 7** Ingawa hana kamanda, ofisa, au mtawala,
- 8** Yeye hutayarisha chakula chake wakati wa kiangazi,^c
Na kukusanya chakula chake wakati wa mavuno.
- 9** Ewe mvivu, utaendelea kulala hapo mpaka lini? Utaamka lini kutoka kati-ka usingizi wako?
- 10** Lala kidogo, sinzia kidogo, Kunja mikono kidogo ili upumzike,^d
- 11** Na umaskini wako utakuja kama jambazi,
Na uhitaji wako kama mwanamume mwenye silaha.^e
- 12** Mtu mwovu asiyefaa kitu huzurura-zurura akisema maneno mapotovu;^f
- 13** Hukonyeza jicho lake,^g hutoa ishara kwa mguu wake, na kuashiria kwa vidole vyake.
- 14** Kwa moyo ulipotoka, Sikuzote anapanga njama

SURA YA 6

a Mt 5:25

b Mt 10:26
Met 26:13-15

c Met 30:24, 25

d Mt 20:13
Met 24:33, 34
Mhu 4:5e Mt 13:4
Met 20:4
Met 24:30-34f Mt 16:27
Yak 3:6g Mt 10:10
Met 16:30

Safu ya 2

a Zb 36:1, 4
Isa 32:7
Mik 2:1b Mt 16:28
Ro 16:17

c Zb 73:12, 18

d Zb 101:5
Met 8:13
Met 16:5e Mt 12:22
Ufu 21:8f Mwa 4:8, 10
Hes 35:31
Kum 27:25g Mt 11:20
Zek 8:17
Mal 2:16

h Kut 23:1

i Law 19:16
Gal 5:20, 21
Yak 3:14, 15j Kum 21:18, 21
Efe 6:1

k Zb 119:105

l Isa 51:4

m Mt 4:13
Ebr 12:11

n Mhu 7:26

o Mt 5:3
Met 7:4, 5za uovu^a na kueneza ugomvi.^b**15** Kwa hiyo, msiba wake utakuja ghafla;Atavunjwa mara moja naye hataweza kupona.^c**16** Kuna vitu sita ambavyo Yehova anachukia;

Naam, vitu saba vinavyomchukiza:

17 Macho ya kiburi,^d ulimi wa uwongo,^e na mikono inayomwaga damu isiyona hatia,^f**18** Moyo unaopanga njama za uovu,^g na miguu inayokimbililia haraka uovu,**19** Shahidi wa uwongo anayesema uwongo kila anapopumua,^hNa mtu yeyote anayepanda ugomvi miongoni mwa ndugu.ⁱ**20** Mwanangu, shika amri ya baba yako,Wala usiyaache mafundisho* ya mama yako.^j**21** Zifunge daima kuzunguka moyo wako;

Zifunge shingoni mwako.

22 Unapotembea huku na huku, itakuongoza; Unapolala, itakulinda; Na unapoamka, itaongea nawe.***23** Kwa maana amri hiyo ni taa,^kNa sheria ni nuru,^lNa makaripio ya nidhamu ndiyo njia ya uzima.^m**24** Yatakulinda dhidi ya mwanamke mwovu,ⁿDhidi ya ulimi unaoshawishi wa mwanamke mwasherati.*^o**6:20** *Au "usiyaache sheria." **6:22** *Au "itakufundisha." **6:24** *Tnn., "mgeni." Angalia Met 2:16.

25 Usiutamani urembo wake moyoni mwako^a

Wala kukubali akunase kwa macho yake yanayo-vutia,

26 Kwa maana kahaba hufanya mtu abaki tu na kipande cha mkate,^b

Lakini mke wa mwanamume mwingine huuwinda uhai wenye* thamani.

27 Je, mtu anaweza kukusanya moto kwenye kifua chake na mavazi yake yasiungue?^c

28 Au je, mtu anaweza kutembea juu ya makaa yanayowaka moto na miguu yake isiungue?

29 Ndivyo ilivyo kwa mtu yeyote anayelala na mke wa jirani yake;

Hakuna yeyote anayemgusa mwanamke huyo atakayekosa kuadhibiwa.^d

30 Watu hawamdharau mwizi Akiiba ili ajishibishe* anapokuwa na njaa.

31 Lakini akipatikana, atalipa mara saba; Atatoa vitu vyote vyenye thamani vya nyumba yake.^e

32 Mtu yeyote anayefanya uzinzi na mwanamke hana busara;*

Yule anayefanya hivyo anajiangamiza mwenyewe.^f

33 Atapata tu majeraha na kuvunjiwa heshima,^g

Na aibu yake haitafutiwa mbali.^h

6:26 *Au "huiwinda nafsi yenye." **6:30** *Au "aijaze nafsi yake." **6:32** *Tnn., "amepungukiwa moyoni."

SURA YA 6

a Mt 5:28
Yak 1:14, 15

b Met 29:3
Lu 15:16, 30

c Gal 6:7

d 2Sa 11:4
2Sa 12:10, 11
Met 6:32-35
Ebr 13:4

e Kut 22:1, 4

f Met 2:18, 19
Met 5:20, 23
Mal 3:5
1Ko 6:9, 10
Ebr 13:4

g Met 5:8, 9

h 1Fa 15:5
1Nya 5:1
Mt 1:6

Safu ya 2

a Mwa 39:19, 20

SURA YA 7

b Met 10:14

c Law 18:5
Kum 5:16
Isa 55:3
Yoh 12:50

d Met 2:10, 11

e Met 23:27, 28

f Met 2:11, 16
Met 5:3
Met 6:23, 24

g Met 6:32
Met 9:16, 17

34 Kwa maana wivu humfanya mume awake hasira; Hataonyesha huruma anapolipiza kisasi.^a

35 Hata kubali fidia* yoyote; Hutamtuliza, hata ukimpa zawadi kubwa kadiri gani.

7 Mwanangu, shika maneno yangu, Na uzihifadhi amri zangu kama hazina.^b

2 Shika amri zangu uishi;^c Linda mafundisho* yangu kama mboni ya jicho lako.

3 Zifunge juu ya vidole vyako;

Ziandike kwenye kibao cha moyo wako.^d

4 Iambie hekima, "Wewe ni dada yangu," Na uuite uelewaji "mtu wangu wa ukoo,"

5 Ili vikulinde dhidi ya mwanamke aliyepotoka,*^e Dhidi ya mwanamke mwasherati* na maneno yake laini.^{#f}

6 Kutoka kwenye dirisha la nyumba yangu, Nilitazama chini kupitia viunzi vya dirisha langu,

7 Na nilipokuwa nikiwachunguza wajinga,* Nilitambua miongoni mwa vijana, kijana fulani mwanamume asiye na busara.^{#g}

8 Alipita barabarani karibu na njia panda anapoishi mwanamke huyo,

6:35 *Au "ridhaa." **7:2** *Au "sheria." **7:5** *Tnn., "mgeni." Angalia Met 2:16. *Au "yenye ushawishi." **7:7** *Au "wasio na uzoefu." #Tnn., "aliyepungukiwa moyoni."

- Naye akashika njia inayoelekea nyumbani kwa mwanamke huyo
- 9** Jioni wakati wa gizagiza,^a Usiku na giza linapoingia.
- 10** Kisha nikamwona mwanamke akiwa kukutana naye, Akiwa amevaa kama* kahaba,^b mwenye moyo mjanja.
- 11** Mwanamke mwenye kelele na mkaidi.^c Hakai* kamwe nyumbani mwake.
- 12** Mara yuko nje, mara yuko katika viwanja vya jiji, Ananyemelea karibu na kila njia panda.^d
- 13** Kisha anamkamata kwa nguvu kijana huyo na kumpiga busu; Bila aibu, mwanamke huyo anamwambia:
- 14** “Nililazimika kutoa dhahabu za ushirika.^e Leo nilitimiza nadhiri zangu.
- 15** Ndiyo sababu nimekuja kukupokea, Kukutafuta, nami nimekupata!
- 16** Nimetandika matandiko bora kitandani mwangu, Kitani cha Misri chenye rangi mbalimbali.^f
- 17** Nimenyunyiza manemane, udi, na mdalasini kitandani mwangu.^g
- 18** Njoo, tunywe na kushiba upendo mpaka asubuhi; Na tujifurahishe kwa mahaaba,
- 19** Kwa maana mume wangu hayuko nyumbani; Amesafiri mbali.

7:10 *Au “Akiwa na mavazi ya.” 7:11 *Tnn., “Miguu yake haikai.”

SURA YA 7

a Ayu 24:15

b Yer 4:30

c Met 9:13-18

d Met 23:27, 28

e Law 19:5

f Eze 27:7

g Wim 3:6
Wim 4:14

Safu ya 2

a Met 5:3

b 1Ko 6:18

c Met 5:8-11

d Met 5:8

e Mhu 7:26

f 1Ko 10:8

SURA YA 8

g Met 1:20, 21

h Mt 10:27

- 20** Alibeba mfuko wa pesa, Naye hatarudi mpaka siku ya mwezi mpevu.”
- 21** Anampotosha kwa ushawishi mkubwa.^a Anamtongoza kwa maneno laini.
- 22** Ghafla kijana huyo anamfuata, kama ng’ombe dume anayeenda machinjioni, Kama mjinga anayeenda kuadhibiwa katika mikatale,^{*b}
- 23** Mpaka mshale unapochocha ini lake; Kama ndege anayekimbia kuingia mtegoni, hajui kwamba hilo litamgharimu uhai wake.^{*c}
- 24** Na sasa, wanangu, nisikilizeni; Sikilizeni kwa makini maneno ninayosema.
- 25** Msiruhusu moyo wenu ugeuke na kufuata njia zake. Msipotee njia na kufuata vijija vyake,^d
- 26** Kwa maana amewaangamiza wengi,^e Na wale aliowaua ni wengi sana.^f
- 27** Nyumba yake huongoza Kaburini;* Hushuka chini kwenye vyumba vya ndani vya kifo.
- 8** Je, hekima haipazi sauti? Je, utambuzi hauinui sauti yake?^g
- 2** Kwenye sehemu zilizoinuka^h pembeni mwa barabara,

7:22 *Au “pingu.” 7:23 *Au “nafsi yake.” 7:27 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

- Husimama kwenye makutano ya barabara.
- 3** Karibu na malango yanayoelekea jijini, Kwenye njia zinazoelekea milangoni, Huendelea kulia kwa sauti kubwa:^a
- 4** “Ninawaita, enyi watu, ninawaita; Ninampazia sauti kila mtu.*
- 5** Enyi wajinga, jifunzeni werevu;^b Enyi wapumbavu, jipatieni moyo wenye uelewaji.*
- 6** Sikilizeni, kwa maana ninayosema ni muhimu, Midomo yangu husema yaliyo sawa;
- 7** Kwa maana kinywa changu husema ukweli kwa sauti ya chini, Na midomo yangu huchukia jambo ovu.
- 8** Maneno yote ya kinywa changu ni ya uadilifu. Hakuna neno hata moja lililopinda wala kupotoka.
- 9** Yote yako wazi kabisa kwa mtu mwenye utambuzi Nayo ni sawa kwa wale ambao wamepata ujuzi.
- 10** Chukueni nidhamu yangu badala ya fedha, Na ujuzi badala ya dhahabu bora zaidi,^c
- 11** Kwa maana hekima ni bora kuliko marijani;* Vitu vingine vyote vinyotamanika haviwezi kulinganishwa nayo.
- 12** Mimi, hekima, ninakaa pamoja na werevu;

8:4 *Au “kila mwanadamu.” 8:5 *Tnn., “eleweni moyo.” 8:11 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 8

a Mdo 20:20

b Zb 19:7

c Zb 19:9,10
Zb 119:72,127
Met 3:13-15

Safu ya 2

a Met 2:11
Met 5:1, 2b Zb 97:10
Zb 101:3
Met 16:6
Ro 12:9c Zb 101:5
1Pe 5:5

d Met 4:24

e Met 2:7

f Met 4:7

g Met 24:5

h Zb 72:1

i Met 2:4, 5

j Met 3:13, 14

k Yoh 1:1-3, 14

l Kol 1:15-17

Nimepata ujuzi na uwezo wa kufikiri.^a

- 13** Kumwogopa Yehova huamaanisha kuchukia uovu.^b Ninachukia kujikweza na kiburi^c na njia ya uovu na maneno mapotovu.^d
- 14** Nina ushauri mzuri na hekima inayotumika;^e Uelewaji^f na nguvu^g ni vyangu.
- 15** Kwa msaada wangu wafalme huendelea kutawala, Na maofisa wakuu hutunga sheria za uadilifu.^h
- 16** Kwa msaada wangu wakuu huendelea kutawala, Na viongozi huhukumu kwa uadilifu.
- 17** Ninawapenda wale wanaonipenda, Na wale wanaonitafuta watanipata.ⁱ
- 18** Nina utajiri na utukufu, Mali inayodumu* na uadilifu.
- 19** Tunda langu ni bora kuliko dhahabu, hata kuliko dhahabu safi, Na mazao yangu ni bora kuliko fedha bora kabisa.^j
- 20** Mimi hutembea katika kijia cha uadilifu, Katikati ya vijia vya haki;
- 21** Mimi huwapa urithi mwingi wale wanaonipenda, Nami huyajaza maghala yao.
- 22** Yehova aliniumba mwanzoni mwa njia yake,^k Mwanzo kabisa wa kazi zake za zamani za kale.^l

8:18 *Au “Kanuni zilizorithiwa.”

- 23** Niliimarishwa tangu nyakati za kale,^a
Tangu mwanzoni, nyakati za mapema kabla ya dunia kuwepo.^b
- 24** Wakati ambapo hakukuwa na vilindi vya maji,^c nilizaliwa,*
Wakati ambapo hakukuwa na chemchemi zilizofurika maji.
- 25** Kabla milima haijawekwa mahali pake,
Kabla ya vilima, nilizaliwa,
- 26** Wakati ambapo hakuwa ameiumba dunia na mashamba yake
Wala mabonge ya kwanza ya udongo.
- 27** Alipozitayarisha mbingu,^d nilikuwepo;
Alipouweka upeo* juu ya maji,^e
- 28** Alipoyafanya imara mawingu yaliyo juu,
Alipojenga msingi wa chemchemi za vilindini,
- 29** Alipoiwekea bahari sheria Kwamba maji yake yasipite agizo lake,^f
Alipoiweka* misingi ya dunia,
- 30** Wakati huo nilikuwa kando yake nikiwa mfanyakazi stadi.^g
Mimi ndiye aliyenipenda sana^h siku baada ya siku; Nilishangilia mbele zake wakati wote;ⁱ
- 31** Nilishangilia dunia yake inayokaliwa,
Nami niliwapenda sana wanadamu.

8:23 *Au "zamani za kale." 8:24 *Au "nilizaliwa kana kwamba kwa chungu wa kuzaa." 8:27 *Tnn., "Alipopiga dua-ra." 8:29 *Au "Alipotunga sheria kuhusu."

SURA YA 8

a Mik 5:2

b Yoh 8:58
Yoh 17:5

c Mwa 1:2

d Zb 33:6
Yer 10:12e Mwa 1:6,7
Ayu 26:10f Ayu 38:8-11
Zb 33:7
Zb 104:6-9
Yer 5:22g Mwa 1:26
Yoh 1:1,3
Yoh 17:5
Kol 1:15,16h Isa 42:1
Mt 3:17

i Ayu 38:7

Safu ya 2

a Met 3:11
Met 4:13
Ebr 12:7,9

b Met 13:14

c Met 5:23

SURA YA 9

d Met 1:20-22

e Zb 119:130

- 32** Na sasa, wanangu, nisikilizeni;
Naam, wenye furaha ni wale wanaoshika njia zangu.
- 33** Sikilizeni nidhamu^a muwe na hekima,
Msiipuuze kamwe.
- 34** Mwenye furaha ni mtu anayenisikiliza
Kwa kuja mapema* milangoni pangu siku baada ya siku,
Kwa kusubiri karibu na miimo ya milango yangu;
- 35** Kwa maana anayenipata mimi atapata uzima,^b
Naye hupata kibali kutoka kwa Yehova.
- 36** Lakini anayenipuuza anajidhuru mwenyewe,*
Na wale wanaonichukia wanapenda kifo."^c
- 9** Hekima ya kweli imejenga nyumba yake;
Imechonga nguzo zake saba.
- 2** Imetayarisha kabisa nyama yake,*
Imechanganya divai yake; Imepanga pia meza yake.
- 3** Imewatuma vijakazi wake Ili waite kwa sauti kutoka vileleni juu ya jiji:^d
- 4** "Yeyote ambaye ni mjinga, na aje humu."
Humwambia yule asiye na busara:*
- 5** "Njoo, ule mkate wangu Na unywe divai niliyochanganya.
- 6** Acha ujinga wako* uishi;^e

8:34 *Au "Kwa kukesha." 8:36 *Au "anaidhuru nafsi yake." 9:2 *Tnn., "Amechinja nyama yake." 9:4 *Tnn., "aliyepungukiwa moyoni." 9:6 *Au "Waache wajinga."

- Tembea moja kwa moja kati-
tika njia ya uelewaji.”^a
- 7** Anayemrekebisha mtu
mwenye dhahaka hualika
aibu,^b
Na yeyote anayemkaripia
mtu mwovu ataumia.
- 8** Usimkaripie mtu mwenye
dhahaka, kwa maana ata-
kuchukia.^c
Mkaripie mwenye hekima,
naye atakupenda.^d
- 9** Mfundishe mwenye heki-
ma, naye atazidi kuwa na
hekima.^e
Mfundishe mwadilifu,
naye atazidi kuelimika.
- 10** Kumwogopa Yehova ndio
mwanzo wa hekima,^f
Na kumjua Aliye Mtakatifu
Zaidi^g ni uelewaji.
- 11** Kwa maana nitafanya siku
zako ziwe nyingi,^h
Na miaka ya maisha yako
itaongezwa.
- 12** Ukipata hekima, unapata
hekima kwa faida yako
mwenyewe,
Lakini ukiwa mwenye dhi-
haka, utaipeba dhahaka
hiyo peke yako.
- 13** Mwanamke mpumbavu
ana kelele.ⁱ
Yeye ni mjinga na hajui
chochote.
- 14** Huketi kwenye mlango wa
nyumba yake
Kwenye kiti sehemu zili-
zoinuka jijini.^j
- 15** Akiwaita kwa sauti wale
wanaopita karibu naye,
Waendao moja kwa moja
kwenye njia yao:
- 16** “Yeyote ambaye ni mjinga,
aje hapa.”
Huwaambia wale wasio na
busara:^{*k}

9:16 *Tnn., “waliopungukiwa moyoni.”

SURA YA 9

- a Met 4:5
Met 13:20
- b Met 15:12
- c 1Fa 21:20, 21
1Fa 22:8
2Nya 25:15, 16
Mt 7:6
- d Zb 141:5
Met 27:6
Met 28:23
- e Met 1:5
Met 15:31
Met 17:10
Met 25:12
- f Zb 111:10
- g 1Nya 28:9
Mt 11:27
Yoh 17:3
- h Kum 6:1, 2
Met 8:35
Met 10:27
- i Met 7:10, 11
- j Met 23:27, 28
- k Met 6:32

Safu ya 2

- a Met 7:18, 19
- b Met 2:18, 19
Met 7:23, 26
Met 23:27, 28

SURA YA 10

- c Met 1:1
- d Met 13:1
Met 27:11
- e Met 11:4
- f Zb 33:18, 19
Zb 37:25
Mt 6:33
- g Met 20:4
Mhu 10:18
- h Met 12:24
Met 13:4
Met 21:5
- i Met 6:6, 9
- j Kut 23:25
Met 28:20
- k Zb 112:6
Mhu 7:1

- 17** “Maji yaliyoibwa ni ma-
tamu,
Na chakula kinacholiwa si-
rini kinapendeza.”^a
- 18** Lakini hawajui kwamba
wale waliokufa ambao
hawana uwezo wako
hapo,
Na kwamba wageni wake
wamo katika vina vya
Kaburi.^{*b}
- 10** Methali za Sulemani.^c
Mwana mwenye hekima
humfanya baba yake
ashangilie,^d
Lakini mwana mpumbavu
ni huzuni kwa mama
yake.
- 2** Hazina zilizopatikana kwa
uovu hazitakuwa na fai-
da yoyote,
Lakini uadilifu ndio
unaookoa kutoka
katika kifo.^e
- 3** Yehova hatamwacha mwa-
dilifu akae njaa,^f
Lakini atawanyima waovu
wanachotamani.
- 4** Mikono milegevu italeta
umaskini,^g
Lakini mikono yenye bidii
huleta utajiri.^h
- 5** Mwana anayetenda kwa
ufahamu hukusanya ma-
zao wakati wa kiangazi,
Lakini mwana anayetenda
kwa aibu analala usingizi
mzito wakati wa ma-
vuno.ⁱ
- 6** Baraka ziko juu ya kichwa
cha mwadilifu,^j
Lakini kinywa cha mwovu
hufunika ukatili.
- 7** Kumbukumbu* ya mwadi-
lifu itabarikiwa,^k

9:18 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi,
uku. 2012. 10:7 *Au “Sifa.”

- Lakini jina la mwovu litaoza.^a
- 8** Mwenye hekima moyoni atakubali mafundisho,^{*b} Lakini mtu anayezungumza maneno ya upumbavu atakanyagiwa chini.^c
- 9** Anayetembea kwa utimilifu atatembea kwa usalama,^d Lakini anayepotosha njia zake atajulikana.^e
- 10** Anayekonyeza jicho lake kwa hila husababisha huzuni,^f Na yule anayezungumza maneno ya upumbavu atakanyagiwa chini.^g
- 11** Kinywa cha mwadilifu ni chemchemi ya uzima,^h Lakini kinywa cha mwovu hufunika ukatili.ⁱ
- 12** Chuki ndiyo inayochochea ugomvi, Lakini upendo hufunika makosa yote.^j
- 13** Hekima hupatikana kwenye midomo ya mtu mwenye utambuzi,^k Lakini fimbo ni kwa ajili wa mgongo wa mtu asiye na busara.^{*l}
- 14** Watu wenye hekima huhifadhi ujuzi kama hazina,^m Lakini kinywa cha mpumbavu hualika maangamizi.ⁿ
- 15** Mali ya^{*} tajiri ni jiji lake lenye ngome. Ufukara wa maskini ndio unaowaangamiza.^o
- 16** Kazi ya mwadilifu huongoza kwenye uzima;

10:8 *Tnn., "amri." 10:13 *Tnn., "aliye-pungukiwa moyoni." 10:15 *Au "Kitu chenye thamani cha."

SURA YA 10

a Zb 9:5

b Kum 4:6
Zb 19:7
Zb 119:34
Zb 119:100

c Met 18:6

d Zb 25:21

e 1Ti 5:24

f Met 6:12, 13

g Met 18:21

h Met 11:30

i Mt 12:35
Yak 3:5j Met 17:9
1Ko 13:4, 7
1Pe 4:8

k Isa 50:4

l Met 26:3

m Met 9:9

n Met 13:3
Met 18:7o Met 19:7
Met 30:8, 9
Mhu 7:12

Safu ya 2

a Mt 7:17

b 1Sa 18:17, 21

c Mhu 5:2

d Zb 39:1
Met 17:27
Met 21:23
Yak 1:19e Met 12:18
Met 16:13

f Yer 3:15

g Ho 4:6

h Kum 8:17, 18
Zb 37:22
1Ti 6:6i Met 2:10, 11
Met 14:9
Met 15:21j Zb 37:4
1Yo 5:14

Lakini mazao ya mwovu huongoza kwenye dhambi.^a

- 17** Anayetii nidhamu ni kijia kinachoelekea kwenye uzima,^{*} Lakini anayepuza karipio huwapotosha wengine.
- 18** Anayeficha chuki yake husema uwongo,^b Na yule anayeeneza habari zinazodhuru^{*} ni mpumbavu.
- 19** Maneno yanapokuwa mengine, makosa hayawezi kuepukwa,^c Lakini yeyote anayedhibiti midomo yake anatenda kwa busara.^d
- 20** Ulimi wa mwadilifu ni kama fedha bora kabisa,^e Lakini moyo wa mwovu una thamani ndogo.
- 21** Midomo ya mwadilifu huwalisha^{*} wengi,^f Lakini wapumbavu hufa kwa sababu ya kukosa ufahamu.^g
- 22** Baraka ya Yehova ndiyo inayomtajirisha mtu,^h Naye haichanganyi na maumivu.^{*}
- 23** Kutenda mambo ya aibu ni kama mchezo kwa mpumbavu, Lakini hekima ni ya mtu mwenye utambuzi.ⁱ
- 24** Anachoogopa mwovu kitamjia; Lakini tamaa ya mwadilifu itatoshelezwa.^j

10:17 *Au labda, "yuko kwenye kijia kinachoelekea kwenye uzima." 10:18 *Au "uvumi unaodhuru." 10:21 *Au "huwaongoza." 10:22 *Au "huzuni; dhiki."

25 Dhoruba ikipita, mwovu hatakuwepo tena.^a
Lakini mwadilifu ni msingi milele.^b

26 Kama siki kwenye meno na moshi machoni, Ndivyo alivyo mtu mvivu kwa yule anayemtuma.*

27 Kumwogopa Yehova hurefusha maisha,^c
Lakini miaka ya waovu itafupishwa.^d

28 Matarajio ya* waadilifu huleta shangwe,^e
Lakini tumaini la waovu litatokomea.^f

29 Njia ya Yehova ni ngome kwa mtu asiye na lawama,^g
Lakini ni maangamizi kwa watenda maovu.^h

30 Mwadilifu hataangushwa kamwe,ⁱ
Lakini waovu hawataendelea kukaa duniani.^j

31 Kinywa cha mwadilifu huzaa* hekima,
Lakini ulimi uliopotoka utaangamizwa.

32 Midomo ya mwadilifu inajua mambo yanayo-
pendeza,
Lakini kinywa cha waovu kimepotoka.

11 Mizani ya uwongo* huchukiza Yehova,
Lakini kipimo sahihi# hufurahisha.^k

2 Kimbelebele kinapokuja, aibu itafuata,^l
Lakini wenye kiasi wana hekima.^m

3 Utimilifu wa wanyoofu ndio unaowaongoza,ⁿ

10:26 *Au "mwajiri wake." 10:28 *Au "Tumaini la." 10:31 *Au "huzaa tunda la." 11:1 *Au "udanganyifu." #Au "jive kamili la kupimia."

SURA YA 10

a Zb 37:10

b Mt 7:24, 25

c Zb 91:15, 16

d Zb 55:23

e Zb 16:9
Ro 12:12

f Met 11:7

g Met 18:10
Isa 40:31

h Ro 2:6-8

i Zb 16:8

j Zb 37:9

SURA YA 11

k Law 19:36

l Met 16:18
Lu 14:8, 9m Mik 6:8
1Pe 5:5n Zb 26:1
Met 13:6

Safu ya 2

a Met 28:18

b Eze 7:19
Mt 16:26

c Mwa 7:1

d 2Sa 17:23
Est 7:10
Met 5:22

e Yer 39:18

f Met 1:32

g Kut 15:9, 10
Lu 12:18-20h Est 7:9
Met 21:18
Da 6:23, 24

i Met 2:10-12

j Kut 15:20, 21
Est 9:19, 22

k Met 14:34

l Yak 3:6

Lakini ujanja wa wenye hila utawaangamiza.^a

4 Mali haitakuwa* na faida yoyote siku ya ghadhabu,^b

Lakini uadilifu ndio utakaoka kutoka katika kifo.^c

5 Uadilifu wa mtu asiye na lawama hukinyoosha kijia chake,

Lakini mwovu ataanguka kwa sababu ya uovu wake mwenyewe.^d

6 Uadilifu wa wanyoofu utawaoka,^e

Lakini wenye hila wata-naswa na tamaa zao wenyewe.^f

7 Mtu mwovu anapokufa, tumaini lake hutokomea; Na matarajio aliyokuwa nayo kwa kutegemea nguvu zake hutokomea pia.^g

8 Mwadilifu huokolewa kutoka katika taabu, Na mwovu huangia humo badala yake.^h

9 Kwa kinywa chake mwasi imani* humwangamiza jirani yake,
Lakini kwa ujuzi waadilifu huokolewa.ⁱ

10 Wema wa watu waadilifu hulifanya jiji lishangilie,
Na waovu wanapoangamia, kunakuwa na kelele za shangwe.^j

11 Jiji hukwezwa kwa sababu ya baraka ya mtu mnyoofu,^k
Lakini kinywa cha waovu hulibomoa.^l

11:4 *Au "Vitu vyenye thamani havitakuwa." 11:9 *Au "mtu anayemkataa Mungu."

- 12** Mtu yeyote asiye na busara* humdharau jirani yake,
Lakini mtu mwenye utambuzi wa kweli hukaa kimya.^a
- 13** Mchungezi huzururazurura akifunua mazungumzo ya siri,^b
Lakini mtu anayeaminika* hutunza siri.[#]
- 14** Mwelekezo stadi* unapokosekana, watu huanguka,
Lakini washauri wengi huleta mafanikio.^{#c}
- 15** Yeyote anayemwekea dhama ya mkopo* mtu asiyemjua hakika atamkia,^d
Lakini yeyote anayeepuka* kumpa mkono ili kumdamini atakuwa salama.
- 16** Mwanamke mwenye fadhili* hupata utukufu,^e
Lakini watu wasio na huruma hujitwalia utajiri.
- 17** Mtu mwenye fadhili* hujinufaisha,^{#f}
Lakini mtu mkatili hujiletea shida.^{△g}
- 18** Mtu mwovu hupata mshahara wa udanganyifu,^h
Lakini mtu anayepanda uadilifu hupata thawabu ya kweli.ⁱ
- 19** Anayetetea uadilifu kwa uthabiti atapata uzima,^j

11:12 *Tnn., "aliyepungukiwa moyoni." 11:13 *Tnn., "mwaminifu roho ni." #Tnn., "hufunika jambo." 11:14 *Au "Mwongozo wenye hekima." #Au "wokovu." 11:15 *Au "rehani." #Tnn., "anayechukia." 11:16 *Au "anayevutia." 11:17 *Au "Mtu mwenye upendo mshikamanifu." #Au "huitendea mema nafsi yake." △Au "aibu."

SURA YA 11

a Met 17:27
1Pe 2:23

b Law 19:16
Met 20:19
Met 26:22

c Met 15:22
Met 20:18
Met 24:6

d Met 6:1, 5
Met 20:16

e 1Sa 25:39
1Pe 3:3, 4

f Lu 6:38

g Yak 5:3, 4

h Ayu 27:13, 14

i Gal 6:7, 8

j Mdo 10:34, 35
Ufu 2:10

Safu ya 2

a Zb 18:26
Met 3:32

b Zb 51:6
Met 15:8

c Mhu 8:13
Eze 18:4

d Isa 26:9
Mt 5:6

e Kum 15:10
Met 19:17
Mhu 11:1, 2

f Hag 1:6

g Mdo 20:35
2Ko 9:6

h Lu 6:38

i Met 12:2

j Est 7:10
Zb 10:2

- Lakini anayefuatia uovu anaelekea kwenye kifo.
- 20** Waliopotoka moyoni wanamchukiza Yehova,^a
Lakini wale ambao njia yao haina lawama humfurahisha.^b
- 21** Uwe na hakika kuhusu hili:* Mtu mwovu hatakosua kuadhibiwa,^c
Lakini watoto wa mwadilifu wataponyoka.
- 22** Kama pete ya dhahabu katika pua ya nguruwe Ndivyo alivyo mwanamke mrembo anayekataa busara.
- 23** Tamaa ya waadilifu huongoza kwenye mema,^d
Lakini tumaini la waovu huongoza kwenye ghadhabu.
- 24** Mtu mmoja hutoa kwa ukarimu* na kupata vitu vingi zaidi;^e
Mtu mwingine huwanyima wengine wanachostahili, lakini anakuwa maskini.^f
- 25** Mtu mkarimu atapata ufanisi,^{*g}
Na yule anayewaburudisha wengine[#] yeye mwenyewe ataburudishwa.^h
- 26** Watu watamlaani anayeficha nafaka,
Lakini watambariki anayeyuza.
- 27** Anayetafuta kwa bidii kutenda mema hutafuta kibali,ⁱ
Lakini anayetafuta uovu —kwa hakika atapatawa na uovu.^j

11:21 *Tnn., "Mkono kwa mkono." 11:24 *Tnn., "hutawanya." 11:25 *Tnn., "atanepeshwa." #Tnn., "anayanyweshwa wengine kwa ukarimu."

28 Anayeutumaini utajiri wake ataanguka,^a
Lakini waadilifu watasita-wi kama majani.^b

29 Yeyote anayewaletea taabu* watu wa nyumbani mwake atarithi upepo,^c
Na mpumbavu atakuwa mtumishi wa mtu mwenye hekima moyoni.

30 Tunda la mwadilifu ni mti wa uzima,^d
Na yule anayeziteka* nafsi# ni mwenye hekima.^e

31 Ikiwa, kwa hakika, mtu mwadilifu duniani huthawabishwa,
Sembuse mwovu na mte-nda dhambi!^f

12 Anayependa nidhamu anapenda ujuzi,^g
Lakini anayechukia kari-pio hana akili.*^h

2 Mtu mwema hupata kibali cha Yehova,
Lakini Yeye humhukumu mtu anayepanga njama za uovu.ⁱ

3 Hakuna mtu anayekuwa salama kwa kutenda uovu,^j
Lakini waadilifu hawata-ng'olewa kamwe.

4 Mke mwema* ni taji kwa mume wake,^k
Lakini mke anayetenda kwa aibu ni kama uozo katika mifupa ya mume wake.^l

5 Mawazo ya waadilifu ni ya haki,
Lakini mwongozo wa wao-vu hudanganya.

11:29 *Au "aibu." 11:30 *Au "anayezishawishi." #Angalia Kamusi, uku. 2012. 12:1 *Au "hana ufahamu." 12:4 *Au "mwenye uwezo."

SURA YA 11

a Ayu 31:24, 28
Zb 52:5, 7

b Zb 1:2, 3
Zb 52:8

c Yos 7:15

d Met 15:4

e 1Ko 9:20-22
Yak 5:19, 20

f Eze 18:24
2Th 1:6
1Pe 4:18

SURA YA 12

g Met 4:13

h Zb 32:9

i Kum 25:1
1Fa 8:31, 32

j Zb 37:10, 38

k Met 18:22
Met 19:14

l 1Fa 21:25

Safu ya 2

a 2Sa 17:1, 2

b Est 7:3, 4
Met 14:3

c Met 24:3
Mt 7:24, 25

d Mwa 41:39
1Sa 16:18

e 1Sa 25:14, 17
Mt 27:3, 4

f Met 13:7

g Mwa 33:12-14
Kut 23:12
Kum 22:4, 10
Kum 25:4
Yon 4:11

h Met 28:19
Efe 4:28

i 1Fa 2:23, 24
Zb 5:6
Mhu 5:6

j Met 13:2
Met 18:20

6 Maneno ya waovu huvizia ili kuua,^{*a}

Lakini kinywa cha wa-nyoofu huwaokoa.^b

7 Waovu wanapoangami-zwa, hawako tena,
Lakini nyumba ya mwadilifu itaendelea kusimama.^c

8 Mtu husifiwa kwa sababu ya busara ya kinywa chake,^d

Lakini mtu aliye na moyo uliopotoka atatendewa kwa dharau.^e

9 Ni afadhali usiheshimiwe sana lakini uwe na mtumishi

Kuliko kujitukuza mwe-nyewe na ukose chakula.*^f

10 Mwadilifu huwatunza wa-nyama anaowafuga,^{*g}
Lakini hata rehema ya waovu ni ukatili.

11 Anayelima shamba lake atakuwa na chakula tele,^h

Lakini anayefuatia vitu vi-sivyo na maana hana busara.*

12 Mtu mwovu hutamani kitu kilichokamatwa na watu wengine waovu,
Lakini mzizi wa waadilifu huzaa matunda.

13 Mwovu hunaswa na mazu-ngumzu yake ya dhambi,ⁱ
Lakini mwadilifu huokoka kutoka katika taabu.

14 Mtu hushiba mema kwa sababu ya matunda ya maneno yake,^{*j}

12:6 *Tnn., "huvizia ili kumwaga damu."

12:9 *Tnn., "mkate." 12:10 *Au "hui-tunza nafsi ya mnyama anayemfuga."

12:11 *Tnn., "amepungukiwa moyoni."

12:14 *Tnn., "kinywa chake."

- Na kazi ya mikono yake itamthawabisha.
- 15** Njia ya mpumbavu ni sawa machoni pake mwe-nyewe,^a
Lakini mwenye hekima hu-kubali ushauri.^{*b}
- 16** Mjinga huonyesha papo hapo* kwamba ameu-dhika,^c
Lakini mtu mwerevu hu-puuza^d matusi.
- 17** Anayetoa ushahidi kwa uaminifu atasema ukweli,^{*}
Lakini shahidi wa uwongo husema mambo ya u-da-nganyifu.
- 18** Maneno yanayosemwa bila kufikiri huchoma kama upanga,
Lakini ulimi wa mwenye hekima huponya.^d
- 19** Midomo inayosema ukweli itadumu milele,^e
Lakini ulimi unaosema uwongo utadumu kwa muda mfupi tu.^f
- 20** Udanganyifu umo moyoni mwa wale wanaopanga njama zinazodhuru,
Lakini wale wanaosita-wisha* amani wana shangwe.^g
- 21** Hakuna madhara yataka-yompata mwadilifu,^h
Lakini waovu watapatwa na misiba mingi.ⁱ
- 22** Midomo inayosema uwongo humchukiza Yehova,^j
Lakini wanaotenda kwa uaminifu humfurahisha.

12:15 *Au "mashauri." 12:16 *Au "siku hiyohiyoi." *Tnn., "hufunika." 12:17 *Tnn., "mambo ya uadilifu." 12:20 *Tnn., "Lakini washauri wa."

SURA YA 12

a Met 3:7
Met 26:12

b Met 1:5

c Met 29:11

d Met 16:24

e 1Pe 3:10

f Met 19:9
Mdo 5:3, 5

g Mt 5:9

h Zb 91:9,10

i Met 1:30, 31
Isa 48:22

j Zb 5:6
Met 6:16, 17
Ufu 21:8

Safu ya 2

a Met 10:19

b Mwa 39:4
1Fa 11:28

c Met 19:15

d Zb 38:6
Met 13:12
Met 15:13

e Met 16:24
Isa 50:4

f Met 26:13-15

g Zb 37:27
Met 10:7
Hab 2:4

SURA YA 13

h Ebr 12:7,9

i 1Sa 2:22-25
Met 9:7

j Met 12:14
Met 18:20

k Zb 39:1
Zb 141:3
Met 21:23

l Met 10:19
Mt 12:36

m Met 26:13-15

- 23** Mtu mwerevu hufunika mambo anayojua,
Lakini moyo wa mjinga hu-bubujika ujinga.^a
- 24** Mkono wa wenye bidii uta-tawala,^b
Lakini mikono milegevu italazimishwa kufanya kazi za utumwa.^c
- 25** Mahangaiko yaliyo moyoni mwa mtu huulemea moyo,^{*d}
Lakini neno jema huucha-ngamsha.^e
- 26** Mwadilifu hutafuta mali-sho yake,
Lakini njia ya waovu hu-wapotosha.
- 27** Watu wavivu hawakimbizi mawindo,^f
Lakini bidii ni hazina ya mtu yenye thamani.
- 28** Kijia cha uadilifu huongo-za kwenye uzima;^g
Kando ya kijia hicho haku-na kifo.

13 Mwana mwenye hekima hukubali nidhamu ya baba yake,^h

Lakini mwenye dhihaka hasikilizi kemeo.^{*i}

2 Mtu atakula mema kwa sababu ya matunda ya maneno yake,^{*j}

Lakini tamaa hasa[#] ya we-nye hila ni ukatili.

3 Anayelinda kinywa chake anaulinda uhai wake,^{*k}

Lakini anayefungua wazi midomo yake ataanga-mia.^l

4 Kuna vitu anavyotamani sana mtu mvivu, ingawa hana chochote,^m

12:25 *Au "humfanya ashuke moyo." 13:1 *Au "rekebisho." 13:2 *Tnn., "kinywa chake." *Au "Lakini nafsi hasa." 13:3 *Au "anailinda nafsi yake."

- Lakini mwenye bidii atato-shelezwa kikamili.*^a
- 5** Mwadilifu huchukua uwo-ngo,^b
Lakini matendo ya waovu huleta aibu na fedheha.
- 6** Uadilifu humlinda mtu ambaye njia yake haina hatia,^c
Lakini uovu humshusha mtenda dhambi.
- 7** Kuna mtu anayejifanya tajiri ingawa hana cho-cho-cho;^d
Kuna mtu anayejifanya maskini ingawa ana mali nyingi.
- 8** Utajiri ni fidia ya uhai wa mtu,^e
Lakini maskini hata hawataishwi.*^f
- 9** Nuru ya waadilifu hung'aa kwa uangavu,*^g
Lakini taa ya waovu itazi-mwa.^h
- 10** Kimbelebele husababi-sha mzozo tu,ⁱ
Lakini hekima ni ya wale wanaotafuta ushauri.*^j
- 11** Mali inayopatikana haraka* itapungua,^k
Lakini mali ya yule anayei-kusanya kidogo kidogo[#] itaongezeka.
- 12** Matarajio yaliyoahiri-shwa* hufanya moyo uwe mgonjwa,^l
Lakini tamaa inayotoshe-lezwa ni mti wa uzima.^m
- 13** Yeyote anayedharau ma-fundisho* atalipia adhabu yake,ⁿ

13:4 *Tnn., "atanenepesha." **13:8** *Tnn., "hawasikii kemeo lolote." **13:9** *Tnn., "hushangilia." **13:10** *Au "wanaoshauriana." **13:11** *Au "Mali inayotokana na ubatili." *Tnn., "anayekusanya kwa mkono." **13:12** *Au "Tumaini lililoahirishwa." **13:13** *Au "neno."

SURA YA 13

a Met 10:4
Met 12:24

b Zb 119:163
Met 8:13
Efe 4:25

c Zb 25:21

d Met 12:9

e Yer 41:8

f Yer 39:10

g Zb 97:11

h Met 24:20

i Amu 8:1

j Met 11:2
Met 24:6
Mdo 15:5, 6

k Met 28:8
Yer 17:11

l Zb 143:7

m Mwa 21:5-7
Lu 2:29, 30

n 2Nya 36:15, 16

Safu ya 2

a Zb 19:8, 11
Met 13:18

b Met 24:14

c Met 14:15

d 1Sa 25:25

e 2Sa 4:9, 10

f Met 25:25

g Zb 141:5
Met 15:32
Ebr 12:11

h 1Fa 1:47, 48

i Amo 5:10

j Mdo 4:13

k Mwa 34:1, 2

l Kum 28:20

m Ro 2:9, 10

n Kum 6:10, 11

- Lakini anayeheshimu amri atathawabishwa.^a
- 14** Mafundisho* ya mwenye hekima ni chemchemi ya uzima^b
Humwepusha mtu na mitego ya kifo.
- 15** Ufahamu ulio makini huleta kibali,
Lakini njia ya wenye hila ni ngumu sana.
- 16** Mtu mwerevu hutenda kwa ujuzi,^c
Lakini mjinga hufunua ujinga wake mwenyewe.^d
- 17** Mjumbe mwovu huanguka taabani,^e
Lakini mjumbe mwaminifu huleta maponyo.^f
- 18** Yeyote anayepuuza nidhamu huwa maskini na kupata aibu,
Lakini anayekubali kure-kebishwa* atatukuzwa.^g
- 19** Tamaa inapotoshezwa ni tamu kwa mtu,*^h
Lakini wapumbavu huchukua kuacha uovu.ⁱ
- 20** Anayetembea na wenye hekima atakuwa na hekima,^j
Lakini anayeshirikiana na wapumbavu ataumia.^k
- 21** Msiba huwafuatia wate-nda dhambi,^l
Lakini ufanisi huwathawabisha waadilifu.^m
- 22** Mtu mwema huwaachia urithi wajukuu wake,
Lakini mali ya mtenda dhambi itaweka akiba kwa ajili ya mwadilifu.ⁿ
- 23** Shamba la maskini lililolimwa huzaa chakula kingi,

13:14 *Au "Sheria." **13:18** *Au "kari-pio." **13:19** *Au "nafsi."

Lakini linaweza* kufagiliwa mbali na ukosefu wa haki.

24 Yeyote anayeizua fimbo yake* anamchukia mwanawe,^a

Lakini yule anayempenda humtia nidhamu kwa bidii.^{#b}

25 Mwadilifu hula na kuto-sheleza hamu* yake,^c

Lakini tumbo la waovu liko tupu.^d

14 Mwanamke ambaye kwa kweli ana hekima huijenga nyumba yake,^e

Lakini aliye mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe.

2 Mtu anayetembea kwa unyoofu wake anamwogopa Yehova,

Lakini yule ambaye njia zake ni zenye hila* humdharau Yeye.

3 Fimbo ya kiburi imo kinywani mwa mpumbavu, Lakini midomo ya wenye hekima itawalinda.

4 Mahali pasipo na ng'ombe, hori ni safi, Lakini nguvu za ng'ombe dume huleta mavuno mengi.

5 Shahidi mwaminifu hata-sema uwongo, Lakini shahidi wa uwongo husema uwongo kila anapopumua.^f

6 Mtu mwenye dhikana hutafuta hekima lakini haipati kamwe, Lakini ujuzi humjia kwa

13:23 *Au "anaweza." 13:24 *Au "asi-yetoa nidhamu; adhabu." #Au lab-da, "bila kukawia." 13:25 *Au "nafsi." 14:2 *Au "zimepotoka."

SURA YA 13

a 1Sa 3:12, 13
1Fa 1:5, 6
Met 29:15

b Kum 6:6, 7
Met 19:18
Met 22:15
Efe 6:4
Ebr 12:6

c Zb 34:10
Zb 37:25

d Isa 65:13

SURA YA 14

e Met 24:3
Met 31:26

f Met 6:16, 19
Met 19:5

Safu ya 2

a Met 18:15

b Met 13:20

c Met 14:12

d Met 10:23
Met 30:20

e Met 21:12

f Met 30:12

g Met 16:25

h Met 1:32

i Gal 6:7, 8

urahisi mtu aliye na uelewaji.^a

7 Kaa mbali na mtu mpumbavu,

Kwa maana hutapata ujuzi katika midomo yake.^b

8 Kwa hekima, mtu mwe-revu huelewa njia anayofuata,

Lakini wapumbavu hudanganywa* na ujinga wao.^c

9 Wajinga hufanyia mzaha hatia,^{*d}

Lakini wanyoofu wako tayari kufanya mapatano.[#]

10 Moyo hujua uchungu wake wenyewe,^{*}

Na hakuna mgeni yeyote anayeweza kushiriki shangwe yake.

11 Nyumba ya mwovu itaharibiwa,^e

Lakini hema la mnyoofu litasitawi.

12 Kuna njia inayoonekana kuwa sawa machoni pa mtu,^f

Lakini mwishowe inaongoza kwenye kifo.^g

13 Hata katika kicheko moyo unaweza kuhisi maumivu,

Na shangwe inaweza kuisia katika huzuni.

14 Mtu aliyepotoka moyoni atavuna matokeo ya njia zake,^h

Lakini mtu mwema huvuna thawabu ya matendo yake.ⁱ

14:8 *Au labda, "wapumbavu huwadanga nganya wengine." 14:9 *Au "hufanya mzaha wanapoambiwa wafanye marekebicho." #Au "Lakini kuna nia njema kati ya wanyoofu." 14:10 *Au "uchungu wa nafsi yake."

- 15** Mjinga* huamini kila neno,
Lakini mwerevu hutafakari kila hatua.^a
- 16** Mwenye hekima hujihadhari na kuepuka uovu,
Lakini mpumbavu hajali,* naye anajiamini kupita kiasi.
- 17** Yule anayekasirika upesi hutenda kipumbavu,^b
Lakini mtu anayechangana mambo* huchukiwa.
- 18** Mjinga* atarithi upumbavu,
Lakini werevu huvikwa ujuzi kama taji.^c
- 19** Watu wabaya watalazimika kuinama chini mbele ya watu wema,
Na waovu watainama katika malango ya waadilifu.
- 20** Maskini huchukiwa hata na majirani zake,^d
Lakini tajiri ana marafiki wengi.^e
- 21** Anayemdharau jirani yake anatenda dhambi,
Lakini yeyote anayewahurumia watu wa hali ya chini ni mwenye furaha.^f
- 22** Je, wale wanaopanga njama zinazodhuru hawatapotea njia?
Lakini wanaokusudia kutenda mema watapata upendo mshikamanifu na uaminifu.^g
- 23** Kila aina ya kazi ngumu ina faida,
Lakini maneno matupu huleta umaskini.^h
- 24** Tajiri la wenye hekima ni mali yao;

14:15, 18 *Au "Asiye na uzoefu." **14:16** *Au "ana hasira kali." **14:17** *Au "mwenye uwezo wa kufikiri."

SURA YA 14

a Ne 6:2, 3
Met 27:12

b Met 12:16
Met 16:32

c Met 4:7-9

d Met 19:7

e Met 19:4

f Zb 41:1
Met 19:17
Isa 58:7, 8

g Ayu 42:10
Zb 25:10

h Met 28:19

Safu ya 2

a Met 27:22

b Zb 34:9
Ro 8:31

c Met 18:10
Yer 15:11

d 1Fa 4:21

e Met 17:27
Yak 1:19

f Met 25:28
Met 29:11
Mhu 7:9

g Mwa 37:3, 4
1Sa 18:8, 9

h Kum 24:14, 15
Zb 12:5

i Mt 19:21

j Met 2:7
Met 10:9

k Met 15:28

- Lakini ujinga wa wapumbavu ni ujinga tu.^a
- 25** Shahidi wa kweli huokoa uhai,*
Lakini shahidi mdanganyifu husema uwongo kila anapopumua.
- 26** Anayemwogopa Yehova humtumaini kwa uthabiti,^b
Na woga huo utakuwa kimbilio kwa watoto wake.^c
- 27** Kumwogopa Yehova ni chemchemi ya uzima,
Humwepusha mtu na mitego ya kifo.
- 28** Umati wa watu ni fahari ya mfalme,^d
Lakini mtawala asiye na raia huangamia.
- 29** Mtu asiyekasirika upesi ana utambuzi mwingi,^e
Lakini asiye na subira hudihihirisha upumbavu.^f
- 30** Moyo mtulivu huupa mwili uzima,*
Lakini wivu huozesha mifupa.^g
- 31** Anayempunja mtu wa hali ya chini anamtukana Muumba wake,^h
Lakini yeyote anayewahurumia maskini humtukua Mungu.ⁱ
- 32** Mtu mwovu ataangamizwa na uovu wake mwenyewe,
Lakini mwadilifu atapata kimbilio katika utimilifu wake.^j
- 33** Hekima hutulia katika moyo wa mtu mwenye uelewaji,^k
Lakini miongoni mwa wapumbavu ni lazima ijitangaze.

14:25 *Au "nafsi." **14:30** *Au "afya."

- 34** Uadilifu hulikweza taifa,^a
Lakini dhambi hulifedhe-
hesha taifa.
- 35** Mfalme hufurahishwa na
mtumishi anayetenda
kwa ufahamu,^b
Lakini hasira yake huwaka
dhidi ya yule anayetenda
kwa aibu.^c
- 15** Jibu la upole* hutuliza
hasira,^d
Lakini neno kali# hucho-
chea hasira.^e
- 2** Ulimi wa mwenye hekima
hutumia vizuri ujuzi,^f
Lakini kinywa cha
mpumbavu hububujika
ujinga.
- 3** Macho ya Yehova yako kila
mahali,
Yakiwaangalia waovu na
wema.^g
- 4** Ulimi mtulivu* ni mti wa
uzima,^h
Lakini maneno yaliyopoto-
ka hukatisha tamaa.[#]
- 5** Mjinga hudharau nidhamu
ya baba yake,ⁱ
Lakini mwerevu hukubali
kurekebishwa.^{*j}
- 6** Nyumba ya mwadilifu ina
hazina tele,
Lakini mazao* ya mwovu
humletea taabu.^k
- 7** Midomo ya wenye hekima
hueneza ujuzi,^l
Lakini moyo wa mpumba-
vu haufanyi hivyo.^m
- 8** Dhabihu ya waovu hu-
mchukiza Yehova,ⁿ
Lakini sala ya wanyoofu
humfurahisha Yeye.^o
- 9** Yehova huchukia njia ya
mwovu,^p

15:1 *Au "tulivu." #Au "linaloumiza."
15:4 *Au "Ulimi unaoponya." #Tnn.,
"huiponda roho." 15:5 *Au "karipio."
15:6 *Au "mapato."

SURA YA 14

- a Kum 4:6
b 2Sa 15:32-34
Met 22:29
c 1Fa 2:44, 46

SURA YA 15

- d Amu 8:2, 3
1Sa 25:32, 33
Met 25:15
e 1Fa 12:14, 16
f Met 16:23
Isa 50:4
g 2Nya 16:9
Zb 11:4
Ebr 4:13
h Met 12:18
Met 16:24
Met 17:27
i 1Sa 2:22-25
j Zb 141:5
Met 13:1
Ebr 12:11
k Yak 5:3, 4
l Zb 37:30
Mt 10:27
m Mt 12:34, 35
n Isa 1:11
o Yak 5:16
1Pe 3:12
1Yo 3:21, 22
p Zb 146:9

Safu ya 2

- a Isa 26:7
b 1Fa 18:17, 18
c Law 26:21
Met 1:32
d Zb 139:8
e Yer 17:10
Ebr 4:13
f Met 9:7
Yoh 3:20
Yoh 7:7
g 2Nya 18:6, 7
h Met 12:25
Met 17:22
i Zb 119:97
Mdo 17:11
j Isa 30:9, 10
k Ayu 3:11
l Mdo 16:23-25
m Zb 37:16
n Met 15:17
o Zb 133:1
p Met 17:1

- Lakini humpenda mtu ana-
yefuatia uadilifu.^a
- 10** Nidhamu huonekana kuwa
mbaya* kwa mtu ana-
yeiacha njia,^b
Lakini yeyote anayechukia
karipio atakufa.^c
- 11** Kaburi* na mahali pa
maangamizi# viko wazi
kabisa machoni pa
Yehova.^d
Sembuse mioyo ya wana-
damu!^e
- 12** Mtu mwenye dhikata
hampendi anayemreke-
bisha.^{*f}
Hatatafuta ushauri kutoka
kwa wenye hekima.^g
- 13** Moyo wenye shangwe hu-
fanya uso uchangamke,
Lakini maumivu ya moyo
huiponda roho.^h
- 14** Moyo wenye uelewaji hu-
tafuta ujuzi,ⁱ
Lakini kinywa cha wapu-
mbavu hula* ujinga.^j
- 15** Siku zote za mtu anayete-
seka ni mbaya,^k
Lakini mtu aliye na moyo
mchangamfu* huwa na
karamu daima.^l
- 16** Ni afadhali kuwa na vi-
chache na kumwogopa
Yehova^m
Kuliko kuwa na mali
nyingi pamoja na maha-
ngaiko.^{*n}
- 17** Ni afadhali kula mboga
za majani mahali penye
upendo^o
Kuliko kula ng'ombe dume
aliyenoneshwa* mahali
penye chuki.^p

15:10 *Au "kali." 15:11 *Au "Sheoli."
Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "na
Abadoni." 15:12 *Au "anayemkaripia."
15:14 *Au "hufuatia." 15:15 *Au "mzu-
ri." 15:16 *Au "vurugu." 15:17 *Tnn.,
"aliyelishwa kwenye hori."

- 18** Mtu mwenye hasira kali huchochea mzozo,^a Lakini mtu asiyekasirika upesi hutuliza ugomvi.^b
- 19** Njia ya mvivu ni kama uzio wa miiba,^c Lakini kijia cha wanyoofu ni kama barabara iliyo-sawazika.^d
- 20** Mwana mwenye hekima humfanya baba yake ashangilie,^e Lakini mtu mpumbavu humdharau mama yake.^f
- 21** Mtu asiye na busara* hufurahia ujinga,^g Lakini mtu mwenye utambuzi huenda mbele moja kwa moja.^h
- 22** Mipango huvunjika watu wasiposhauriana,* Lakini mambo hufanikiwa kupitia washauri wengi.ⁱ
- 23** Mtu hushangilia anapotoa jibu linalofaa,*^j Na neno linalosemwa wakati unaofaa—ni jema sana!^k
- 24** Kwa mwenye ufahamu kijia cha uzima huelekea juu,^l Ili kumwepusha na Kaburi* lililo chini.^m
- 25** Yehova ataibomoa nyumba ya mtu mwenye kiburi,ⁿ Lakini ataulinda mpaka wa mjane.^o
- 26** Yehova huchukia njama za mtu mwovu,^p Lakini maneno yanayope-ndeza ni safi Kwake.^q
- 27** Mtu anayepata faida isiyo

15:21 *Tnn., "aliyepungukiwa moyoni."
 15:22 *Au "watu wasipokuwa na mazungumzo ya siri." 15:23 *Tnn., "hushangilia jibu la kinywa chake." 15:24 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 15

- a Met 10:12
 b Mwa 13:8, 9
 1Sa 25:23, 24
 Met 25:15
 Yak 1:19
 c Met 26:13-15
 d Isa 30:21
 e Met 27:11
 f Met 23:22
 Met 30:17
 g Met 26:18, 19
 Mhu 7:4
 h Met 10:23
 Efe 5:15, 16
 Yak 3:13
 i Met 20:18
 j Efe 4:29
 k 1Sa 25:32, 33
 Met 25:11
 l Mt 7:13, 14
 m Met 8:35, 36
 n Lu 18:14
 o Zb 146:9
 p Met 6:16, 18
 q Zb 19:14

Safu ya 2

- a Kum 16:19
 1Sa 8:1, 3
 Met 1:19
 b Isa 33:15, 16
 c Met 16:23
 d Zb 34:15, 16
 Zb 138:6
 Zb 145:19
 Yoh 9:31
 e Met 16:24
 Met 25:25
 f Met 9:8
 Met 19:20
 g Met 5:12, 14
 Ebr 12:25
 h Met 13:18
 Mt 7:24, 25
 i Zb 111:10
 j Met 18:12
 Yak 4:10

SURA YA 16

- k Yer 1:9
 Lu 12:11, 12
 l 1Sa 15:13, 14
 Zb 36:1, 2
 Met 21:2
 Yer 17:9

- ya haki huwaletea taabu* watu wa nyumba yake mwenyewe,^a Lakini anayechukia rushwa ataendelea kuishi.^b
- 28** Moyo wa mwadilifu hutafakari kabla ya kujibu,^c Lakini kinywa cha waovu hububujika mambo mabaya.
- 29** Yehova yuko mbali sana na waovu, Lakini huisikia sala ya waadilifu.^d
- 30** Macho yanayong'aa* hufanya moyo ushangilie; Habari njema huitia nguvu mifupa.^{#e}
- 31** Mtu anayesikiliza karipio la uzima Hutulia miongoni mwa wenyewe hekima.^f
- 32** Yeyote anayekataa nidhamu anaudharau uhai wake,^{#g} Lakini yeyote anayesikiliza karipio hupata uelewaji.^{#h}
- 33** Kumwogopa Yehova ni mazoezi ya kupata hekima,ⁱ Na kabla ya utukufu kuna unyenyekevu.^j

- 16** Mtu huyatayarisha mawazo ya moyo wake,* Lakini jibu analotoa# hutoka kwa Yehova.^k
- 2** Njia zote za mwanadamu huonekana kuwa sawa* machoni pake,^l

15:27 *Au "aibu." 15:28 *Au "hufikiria kwa uangalifu jinsi ya kujibu; hufikiria kabla ya kuongea." 15:30 *Au "Kumtupia mtu jicho kwa uchangamfu." #Tnn., "huienepesha mifupa." 15:32 *Au "anaidharau nafsi yake." #Tnn., "moyo." 16:1 *Tnn., "Mipangilio ya moyo ni ya mtu." #Au "jibu linalofaa." #Tnn., "jibu la ulimi." 16:2 *Tnn., "safi."

- Lakini Yehova huchunguza nia. ^a
- 3** Mkabidhi Yehova lolote unalofanya, ^{a,b}
Na mipango yako itafanikiwa.
- 4** Yehova amefanya kila kitu kitimize kusudi lake, Hata waovu kwa ajili ya siku ya msiba. ^c
- 5** Kila mtu mwenye kiburi moyoni humchukiza Yehova. ^d
Uwe na hakika kwamba* hatakosu kuadhibiwa.
- 6** Kwa upendo mshikamani-fu na uaminifu, kosa husamehewa, ^e
Na kwa kumwogopa Yehova mtu hujiepusha na uovu. ^f
- 7** Yehova anapofurahia njia za mtu,
Huwafanya hata maadui wake wawe na amani naye. ^g
- 8** Afadhali kuwa na kidogo pamoja na uadilifu ^h
Kuliko kuwa na mapato mengi pasipo haki. ⁱ
- 9** Mtu anaweza kupanga njia yake moyoni mwake,
Lakini Yehova ndiye anayezielekeza hatua zake. ^j
- 10** Uamuzi ulioongozwa na roho* unapaswa kuwa katika midomo ya mfalme; ^k
Hapaswi kamwe kusaliti haki. ^l
- 11** Mizani na vipimo vya unyooftu hutoka kwa Yehova;
Mawe yote ya kupimia

16:2 *Tnn., "huzichunguza roho." **16:3** *Tnn., "Mvingirishie Yehova kazi zako." **16:5** *Tnn., "Mkono kwa mkono." **16:10** *Au "Uamuzi ulioongozwa na Mungu."

SURA YA 16

- a 1Sa 16:6,7
Met 24:12
- b Zb 37:5
Flp 4:6,7
- c Kut 14:4
Ro 9:21
- d Met 6:16,17
Met 8:13
Met 21:4
- e Mdo 3:19
- f Ne 5:8,9
2Ko 7:1
- g Mwa 31:24
Kut 34:24
- h ITi 6:6
- i Zb 37:16
Yer 17:11
- j Met 16:1
Yer 10:23
- k Kum 17:18,19
1Fa 3:28
- l Zb 72:1,14
- Safu ya 2**
- a Law 19:36
Met 11:1
- b Met 20:26
- c Met 29:14
Ufu 19:11
- d Zb 101:6
- e 1Sa 22:17,18
1Fa 2:29
- f Mhu 10:4
- g Zb 72:1,6
- h Mhu 7:12
- i Met 4:7
- j Met 10:9
- k Met 11:2
Da 4:30-32
- l Isa 57:15

- yaliyo katika mfuko ni kazi yake. ^a
- 12** Matendo maovu huwachukiza wafalme, ^b
Kwa maana kiti cha ufalme huimarishwa kabisa kwa uadilifu. ^c
- 13** Maneno ya uadilifu huwafurahisha wafalme.
Wanampenda mtu anayeo- ngea kwa unyooftu. ^d
- 14** Ghadhabu ya mfalme ni kama mjumbe wa kifo, ^e
Lakini mtu mwenye hekima huituliza. ^f
- 15** Katika nuru ya uso wa mfalme kuna uzima;
Kibali chake ni kama wingu la mvua wakati wa masika. ^g
- 16** Jinsi lilivyo jambo bora kupata hekima kuliko dhahabu! ^h
Ni bora kuchagua uelewaji kuliko fedha. ⁱ
- 17** Barabara kuu ya wanyooftu huepuka uovu.
Yeyote anayelinda njia yake huhifadhi uhai wake. ^j
- 18** Kiburi hutangulia kuanguka kwa kishindo,
Na roho ya majivuno hutangulia kujikwaa. ^k
- 19** Ni afadhali kuwa mnyenyekevu*^l miongoni mwa wapole
Kuliko kugawana nyara na watu wenye kiburi.
- 20** Mtu anayeonyesha ufahamu katika jambo atapata mafanikio, ^m
Na mwenye furaha ni yule anayemtumaini Yehova.
- 21** Watu wenye hekima moyo-

16:14 *Au "huiepuka." **16:17** *Au "nafsi yake." **16:19** *Tnn., "na roho ya upole." **16:20** *Tnn., "mema."

- ni wataitwa watu wenye uelewaji,^a
Na mtu anayeongea kwa fadhili* huongeza ushawishi.^b
- 22** Ufahamu ni chemchemi ya uzima kwa walio nao, Lakini wajinga hutiwa nidhamu kwa ujinga wao wenyewe.
- 23** Moyo wa mwenye hekima hukipatia kinywa chake ufahamu^c
Na huongeza ushawishi kwenye maneno yake.
- 24** Maneno yanayopendeza ni sega la asali,
Ni matamu kwa nafsi* nayo huponya mifupa.^d
- 25** Kuna njia inayoonekana kuwa sawa machoni pa mtu,
Lakini mwishowe inaongoza kwenye kifo.^e
- 26** Hamu ya chakula* ya mfanyakazi humfanya afanye kazi kwa bidii
Kwa sababu njaa yake^f humchochea kuendelea kufanya kazi.^f
- 27** Mtu asiyefaa kitu huchimbia lililo ovu;^g
Na maneno yake ni kama moto unaounguzi.^h
- 28** Mfanya fujo* husababisha mgawanyiko,ⁱ
Na mchongezi huwateanganisha marafiki wa karibu.^j
- 29** Mtu mkatili humshawishi jirani yake
Na kumwongoza katika njia isiyofaa.

16:21 *Au "Na maneno yanayovutia." Tnn., "Na utamu wa midomo." **16:24** *Au "Yana ladha tamu." Angalia Kamusi, uku. 2012. **16:26** *Au "Nafsi." #Tnn., "mdomo wake." **16:28** *Au "Mpanga njama."

SURA YA 16

a Met 4:7

b Lu 4:22
Kol 4:6c Met 22:17, 18
Mt 12:35d Met 4:20-22
Met 12:18e Met 14:12
Mt 7:22, 23

f Mhu 6:7

g Met 6:12, 14

h Yak 3:6

i Yak 3:16

j Mwa 3:1
1Sa 24:9
Ro 16:17

Safu ya 2

a Law 19:32
Ayu 32:7
Met 20:29

b Zb 92:12-14

c Met 14:29
Yak 1:19

d Met 25:28

e Hes 26:55
Met 18:18f 1Sa 14:41, 42
Mdo 1:24, 26

SURA YA 17

g Zb 37:16

h Met 15:16, 17
Met 21:9, 19

i Met 27:21

j Zb 26:2
Met 21:2
Met 24:12

k Yer 5:31

l Met 14:31

- 30** Hukonyeza jicho lake anapopanga njama zinazodhuru.
Huibanabana midomo yake pamoja anapotekeleza hila.
- 31** Mvi ni taji la umaridadi*^a
Zinapopatikana katika njia ya uadilifu.^b
- 32** Mtu asiyekasirika upesi^c
ni bora kuliko mwana-mume mwenye nguvu,
Na mtu anayedhibiti hasira yake* ni bora kuliko mtu anayelishinda jiji.^d
- 33** Kura hugigwa mapajani,^e
Lakini kila uamuzi unao-fanywa kwa kura hiyo hutoka kwa Yehova.^f

17 Ni afadhali kipande kikavu cha mkate mahali penye amani*^g

Kuliko nyumba iliyojaa karamu[#] pamoja na ugomvi.^h

- 2** Mtumishi mwenye ufahamu atamtawala mwana anayetenda kwa aibu; Atapokea urithi kama ndugu za mwana huyo.
- 3** Chungu cha kusafishia ni kwa ajili ya fedha na tanuru ni kwa ajili ya dhahabu,ⁱ
Lakini Yehova ndiye mchunguzaji wa mioyo.^j
- 4** Mtu mwovu husikiliza maneno yanayoumiza,
Na mtu mdanganyifu husikiliza ulimi unaodhuru.^k
- 5** Yeyote anayemdhihak maskini anamtukana Muumba wake,^l
Na yeyote anayeshangilia

16:31 *Au "utukufu." **16:32** *Tnn., "anayetawala roho yake." **17:1** *Au "utulivu." #Tnn., "dhabihu."

msiba wa mwingine hatakosa kuadhibiwa.^a

6 Wajukuu ni taji kwa waliozeeka,

Na akina baba* ni utukufu wa wana[#] wao.

7 Maneno manyoofu* haya-mfai mpumbavu.^b

Sembuse maneno ya uwongo kwa mtawala!^{#c}

8 Zawadi ni kama kito chenye thamani kwa* aliye nayo;^d

Humletea mafanikio, kila mahali anapoenda.^e

9 Yeyote anayesamehe* kosa hutafuta upendo,^f

Lakini yule anayeendelea kuongea kuhusu jambo huwatenganisha marafiki wa karibu.^g

10 Kemeo humgusa moyo zaidi mtu mwenye uelewaji^h

Kuliko kumpiga mpumbavu mara mia moja.ⁱ

11 Mtu mwovu hutafuta uasi tu,

Lakini mjumbe mkatili atatumwa kumwadhibu.^j

12 Ni afadhali kukutana na dubu aliyenyang'anywa watoto wake

Kuliko kukutana na mtu mpumbavu katika ujinga wake.^k

13 Mtu yeyote akilipa uovu kwa wema,

Uovu hautaondoka katika nyumba yake.^l

14 Kuanzisha vita ni kama kufungua lango la mafuriko;*

17:6 *Au "wazazi." #Au "watoto."

17:7 *Au "mazuri." #Au "kiongozi."

17:8 *Au "ni kito kinachomletea kibali."

17:9 *Tnn., "anayefunika."

17:14 *Au "kufungulia maji bwawani." Tnn., "kufungulia maji."

SURA YA 17

a Met 24:17
Oba 12

b Met 26:7

c Met 16:10

d Mwa 32:20
2Sa 16:1

e 1Sa 25:18, 35
Met 18:16
Met 19:6

f Met 10:12
1Pe 4:8

g Met 16:28

h Zb 141:5
Met 9:8

i Met 27:22

j 2Sa 18:15
2Sa 20:1, 22
1Fa 2:22, 24

k Met 27:3

l 2Sa 12:8-10

Safu ya 2

a Mwa 13:8, 9
Met 25:8
Mt 5:39
Ro 12:18

b Kut 23:7
1Fa 21:13
Isa 5:22, 23

c Met 1:22
Ro 1:20, 21

d Met 18:24
Yoh 15:13

e Ru 1:16, 17
1Sa 19:2

f Met 11:15
Met 22:26, 27

g Yak 3:16

h 2Sa 15:2-4

i Zb 18:26
Met 6:14, 15

j 1Sa 2:22-25
1Sa 8:1-3
2Sa 15:14

k Met 12:25
Met 15:13

l Met 18:14

Kabla ugomvi haujalipuka, ondoka.^a

15 Yeyote anayetangaza kwamba mwovu hana hatia na yeyote anayemshutumu mwadilifu^b

—Wote wawili wanamchukiza Yehova.

16 Kuna faida gani kwa mpumbavu kuwa na uwezo wa kupata hekima

Ilhali hana moyo wa kupata?^{#c}

17 Rafiki wa kweli hupenda nyakati zote^d

Naye ni ndugu ambaye amezaliwa kwa ajili ya nyakati za taabu.^e

18 Mtu ambaye hana busara* humpa mwingine mkono na kukubali

Kuweka dhamana mbele ya jirani yake.^f

19 Mtu anayependa ugomvi anapenda dhambi.^g

Yeyote anayeliinua juu lango lake anaalika msiba.^h

20 Mtu aliyepotoka moyoni hatapata mafanikio,^{*i}

Na yule anayesema maneno ya udanganyifu ataanguka kwenye maangamizi.

21 Baba anayezaa mtoto mpumbavu atahuzunika;

Na baba ya mtoto asiye na akili hana shangwe.^j

22 Moyo wenye shangwe ni dawa nzuri,^{*k}

Lakini roho iliyopondeka humfyonza mtu nguvu.^{#l}

17:16 *Au "Ilhali hana busara?"

17:18 *Tnn., "aliyepungukiwa moyoni."

17:20 *Tnn., "mema."

17:22 *Au "humsaidia mtu kupona." #Au "huikausha kabisa mifupa."

23 Mtu mwovu atachukua ru-shwa kwa siri*

Ili apotoshe njia ya haki.^a

24 Hekima iko mbele kabisa ya uso wa mtu mwenye utambuzi,

Lakini macho ya mpumbavu hutangatanga mpaka kwenye miisho ya dunia.^b

25 Mwana mpumbavu humle-tea huzuni baba yake

Na kumletea maumivu ya moyo* yule aliyemzaa.^c

26 Si vema kumwadhibu* mwadilifu,

Na kuwapiga viboko watu wanaoheshimiwa si jambo linalofaa.

27 Mtu mwenye ujuzi huya-zuia maneno yake,^d

Na mtu mwenye utambuzi atabaki mtulivu.^{*e}

28 Hata mjinga anayekaa ki-mya ataonwa kuwa mwenye hekima,

Na yule anayefunga mido-mo yake, ataonwa kuwa mwenye utambuzi.

18 Yeyote anayejitenga na wengine anafuatia ta-maa zake mwenyewe za kichoyo;

Hukataa* hekima yote ina-yotumika.

2 Mtu mpumbavu hapende-zwi na uelewaji;

Anaona ni afadhali afunue yaliyo moyoni mwake.^f

3 Mtu mwovu anapokuja, dharau huja pia,

Na aibu huja pamoja na fe-dheha.^g

17:23 *Tnn., "rushwa kutoka kifuani."

17:25 *Tnn., "Na kumletea uchungu."

17:26 *Au "kumtoza faini." 17:27

*Tnn., "atabaki na roho iliyotulia." 18:1

*Au "Hudharau."

SURA YA 17

a Kut 23:8

b Mhu 2:14

c Met 15:20

d Met 10:19

Yak 1:19

e Met 15:4

Mhu 9:17

Yak 3:13

SURA YA 18

f Met 10:19

g Met 11:2

Safu ya 2

a Met 10:11

b Kum 1:16, 17

Met 28:21

c 1Fa 21:9, 10

d Met 13:10

e Met 19:19

f Met 13:3

g Law 19:16

h Met 26:22

i Met 10:4

j 1Sa 17:45, 46

Zb 20:1

k Zb 18:2

Zb 91:14

l Zb 49:6, 7

Met 11:4

Yer 9:23

Lu 12:19-21

m Met 11:2

Da 5:23, 30

Mdo 12:21-23

n Met 22:4

1Pe 5:5

o Met 25:8

4 Maneno ya kinywa cha mtu ni maji yenye kina.^a Chemchemi ya hekima ni kijito kinachobubujika.

5 Si vema kumpendelea mwovu^b

Wala kumnyima haki mtu mwadilifu.^c

6 Maneno ya mpumbavu hu-sababisha ugomvi,^d Na kinywa chake hualika kipigo.^e

7 Kinywa cha mpumbavu ndicho kinachomwanga-miza,^f

Na midomo yake ni mtego kwa uhai wake.*

8 Maneno ya mchongezi ni kama matonge matamu;^{*g}

Humezwa na kushuka tu-
mboni moja kwa moja.^h

9 Yeyote aliyे mvivu katika kazi yake Ni ndugu ya mtu mhari-bifu.ⁱ

10 Jina la Yehova ni mnara wenye nguvu.^j

Mwadilifu hukimbilia humo na kupata ulinzi.^{*k}

11 Mali ya tajiri ni jiji lake le-nye ngome;

Ni kama ukuta wa ulinzi katika mawazo yake.^l

12 Kabla ya kuanguka kwa kishindo moyo wa mtu huwa na kiburi,^m

Na kabla ya utukufu kuna unyenyekevu.ⁿ

13 Yeyote anayejibu kabla ya kusikia ukweli wa mambo,

Huo ni upumbavu na aibu kwake.^o

18:7 *Au "nafsi yake." 18:8 *Au "vitu vinavyomezwa kwa pupa." 18:10 *Tnn., "na kuinuliwa juu," yaani, hawezi kufikiwa, yuko salama.

- 14** Roho ya mtu inaweza kumtegemeza anapokuwa mgonjwa,^a
Lakini ni nani anayeweza kustahimili roho iliyopondeka?²*^b
- 15** Moyo wa mtu mwenye uelewaji hupata ujuzi,^c
Na sikio la mwenye hekima hujitahidi kupata ujuzi.
- 16** Zawadi ya mwanadamu humfungulia njia;^d
Humwezesha kufika mbele ya watu mashuhuri.
- 17** Mtu wa kwanza kuwasilisha kesi yake huonekana kuwa sahihi,^e
Mpaka mwingine anapokuja na kumuuliza maswali.*^f
- 18** Kupiga kura hukomesha mizozo^g
Na kukata maneno kati ya wapinzani wenye nguvu.
- 19** Ndugu aliyekosewa ni mgumu kuliko jiji lenye ngome,^h
Na kuna mizozo ambayo ni kama makomeo ya ngome.ⁱ
- 20** Tumbo la mtu litajazwa matunda ya maneno yake;^{*j}
Atashiba mazao ya midomo yake.
- 21** Kifo na uhai viko katika nguvu za ulimi;^k
Wale wanaopenda kuutumia watakula matunda yake.^l
- 22** Anayepata mke mwema amepata kitu chema,^m

18:14 *Au "iliyokata tamaa kabisa?"
18:17 *Au "kumhoji." 18:18 *Tnn., "Na kuwataniganisha." 18:20 *Tnn., "kinywa chake."

SURA YA 18

a Ayu 1:21
2Ko 4:16
2Ko 12:10

b Met 17:22

c 1Fa 3:7-9
Met 9:9

d Mwa 43:11
Met 17:8

e 2Sa 16:3, 4

f 2Sa 19:25-27
Met 25:8

g Yos 14:1, 2
Ne 11:1
Met 16:33

h Mwa 27:41
2Sa 13:22

i 2Sa 14:28
Mdo 15:37-39

j Met 12:14
Met 13:2

k Mt 15:18
Efe 4:29
Yak 3:6, 9

l Mhu 10:12

m Met 31:10

Safu ya 2

a Met 19:14
Mhu 9:9

b 2Sa 15:31
Mt 26:49

c 1Sa 19:2, 4
Met 17:17

SURA YA 19

d Met 15:16
Yak 2:5

e Met 28:6

f Ro 10:2

g Met 14:20

h Kum 19:18, 19

i Met 19:9

j Met 14:20

k Mhu 9:14, 15
Yak 2:2, 3

Naye hupata kabali cha*
Yehova.^a

- 23** Maskini husihi anapoo-
ngea,
Lakini tajiri hujibu kwa
ukali.

- 24** Kuna marafiki walio tayari
kuangamizana,^b
Lakini kuna rafiki anayeshikamana na mtu kwa
ukaribu kuliko ndugu.^c

19 Ni afadhali kuwa maskini
na kutembea kwa
utumilifu^d

Kuliko kuwa mpumbavu
na kusema uwongo.^e

- 2** Mtu asiye na ujuzi si mtu
mzuri,^f

Na mtu anayetenda bila
kufikiri* anatenda dhambi.

- 3** Ujinga wa mtu ndio unapotosha njia yake,
Kisha moyo wake unamkasirikia vikali Yehova.

- 4** Mali huwavuta marafiki
wengi,

Lakini maskini ataachwa
hata na rafiki yake.^g

- 5** Shahidi anayesema
uwongo hatakosa kuadhibiwa,^h

Na yule anayesema uwongo
kila anapopumua hataponyoka.ⁱ

- 6** Wengi hujipendekeza kwa
mtu maarufu,*

Na kila mtu ni rafiki ya
yule anayetoa zawadi.

- 7** Ndugu wote wa mtu maskini humchukia;^j

Marafiki zake humwepuka
hata zaidi!^k

Huwafuatia ili awasihi,

18:22 *Au "nia njema ya." 19:2 *Tnn., "anayetembea haraka." 19:6 *Au "mkarimu."

lakini hakuna yeyote
anayemsikiliza.

- 8** Yeyote anayepata busara*
anajipenda mwenyewe.^{#a}

Yeyote anayethamini uta-
mbuzi kama hazina
atapata mafanikio.^{Δb}

- 9** Shahidi anayesema
uwongo hatakosa
kuadhibiwa,
Na yule anayesema uwo-
ngo kila anapopumua
ataangamia.^c

- 10** Mjinga hastahili kuishi
maisha ya anasa;
Sembuse mtumishi kuwa-
tawala wakuu!^d

- 11** Ufahamu wa mtu hakika
hutuliza hasira yake,^e
Na ni fahari kwake kuachi-
lia* kosa.^f

- 12** Ghadhabu ya mfalme ni
kama mngurumo wa
simba,^{*g}

Lakini kibali chake ni
kama umande juu ya
majani.

- 13** Mwana mpumbavu humle-
tea shida baba yake,^h
Na mke mgomvi* ni kama
paa ambalo haliachi ka-
mwe kuvuja.ⁱ

- 14** Nyumba na mali hurithiwa
kutoka kwa akina baba,
Lakini mke mwenye busa-
ra hutoka kwa Yehova.^j

- 15** Uvivu huleta usingizi
mzito,
Na mtu mzembe atakaa
njaa.^k

- 16** Anayeshika amri anauli-
nda uhai wake,^{*l}

19:8 *Tnn., "moyo." #Au "anaipenda
nafsi yake." ΔTnn., "mema." 19:11
*Tnn., "kupita." 19:12 *Au "mwanasi-
mba mwenye manyoya marefu shingo-
ni." 19:13 *Au "msumbufu." 19:16
*Au "anailinda nafsi yake."

SURA YA 19

a Met 15:32

b Met 2:2, 5

c Met 19:5
Ufu 21:8

d 2Sa 3:24
2Sa 3:38, 39
Met 30:21, 22
Mhu 10:7

e Met 14:29
Met 16:32
Yak 1:19

f Mwa 50:19-21
Mt 18:21, 22
Efe 4:32

g Met 16:14
Met 20:2
Da 2:12

h 2Sa 16:21, 22

i Met 21:9, 19
Met 27:15

j Mwa 24:14
Met 18:22
Met 31:10

k Met 23:21
Met 24:33, 34
2Th 3:10

l Met 16:17

Safu ya 2

a Met 15:32

b Kum 15:7, 8
Zb 37:25, 26
Ebr 13:16

c Met 11:24
Mt 5:7
Ebr 6:10

d Met 13:24
Met 22:6, 15

e 1Sa 3:12, 13

f 1Sa 24:16-18
1Sa 26:21

g Met 4:13

h Kum 8:14, 16
Ebr 12:7, 11

i Mwa 11:6, 7
Mwa 50:19, 20
Met 21:30
Da 4:35
Mdo 5:38, 39

j Mik 6:8

k Met 14:27
Mal 3:16

l Met 12:21

m Met 6:9-11
Met 15:19
Met 24:30, 31
Met 26:14, 15

Asiyejali njia zake
atakufa.^a

- 17** Anayemwonyesha kibali
mtu wa hali ya chini ana-
mkopesha Yehova,^b

Naye Atamlipa* kwa ana-
yotenda.^c

- 18** Mtie nidhamu mtoto*
wako wakati bado kuna
tumaini,^d

Nawe usiwajibike kwa*
kifo chake.^e

- 19** Mtu mwenye hasira kali
atalipia adhabu;

Ukijaribu kumwoko, uta-
lazimika kufanya hivyo
tena na tena.^f

- 20** Sikiliza mashauri na uku-
bali nidhamu,^g

Ili uwe na hekima wakati
wako ujao.^h

- 21** Moyo wa mwanadamu una
mipango mingi,
Lakini shauri* la Yehova
ndilo litakalodumu.ⁱ

- 22** Kinachomfanya mtu awe
mwenye kutamani ni
upendo wake mshikama-
nifu;^j

Na ni afadhali kuwa maski-
ni kuliko kuwa mwongo.

- 23** Kumwogopa Yehova huo-
ngoza kwenye uzima;^k

Yule aliye na woga huo
atakuwa na pumziko
jema, hatapatwa na ma-
dhara.^l

- 24** Mvivu huutumbukiza*
mkono wake katika ba-
kuli la karamu,

Lakini hata hashughuliki
kuurudisha kinywani
mwake.^m

19:17 *Au "Atamthawabisha." 19:18
*Au "mwana." #Au "usitamani."
19:21 *Au "kusudi." 19:24 *Tnn., "huu-
zika."

- 25 Mpige mwenye dhihaka,^a ili mjinga awe mwerevu,^b Mkaripie mwenye uelewaji ili aongeze ujuzi wake.^c
- 26 Yule anayemtendea vibaya baba yake na kumfukuza mama yake Ni mwana anayeleta aibu na fedheha.^d
- 27 Mwanangu, ukiacha kusi-kiliza nidhamu, Utatangatanga mbali na maneno ya ujuzi.
- 28 Shahidi asiyefaa kitu hu-dhihaki haki,^e Na kinywa cha waovu hu-bugia uovu.^f
- 29 Hukumu inawangojea wa-dhihaki,^g Na mgongo wa wapumba-vu unangojea mapigo.^h
- 20** Divai ni mdhihakia,ⁱ ki-
leo ni vurugu;^j
Yeyote anayepotoshwa navyo hana hekima.^k
- 2 Kutisha* kwa mfalme ni kama mngurumo wa simba;^{#l}
Yeyote anayemkasirisha anauhatarisha uhai wake mwenyewe.^m
- 3 Ni heshima kwa mtu kujie-pusha na ugomvi,ⁿ Lakini kila mjinga atajitu-mbukiza humo.^o
- 4 Mvivu halimi katika maji-
ra ya baridi kali,
Kwa hiyo atakuwa akio-mbaomba wakati wa mavuno, wakati hana chochote.*^p
- 5 Mawazo* yaliyo moyoni

20:2 *Au "Kuogopesha." #Au "mwana-simba mwenye manyoya marefu shingoni." 20:4 *Au labda, "Atatazama wakati wa mavuno lakini hatapata chochote." 20:5 *Au "Makusudio." Tnn., "Mashauri."

SURA YA 19

a Kum 25:2

b Met 15:5

c Met 9:9
Met 21:11d Kut 20:12
Law 20:9
Met 20:20
Met 30:17

e 1Fa 21:9,10

f Met 4:16,17

g Met 9:12

h Met 10:13
Met 26:3

SURA YA 20

i Mwa 9:20, 21
Met 23:29-35

j Isa 28:7

k 1Ko 6:10
Gal 5:21
Efe 5:18l Met 19:12
Mhu 10:4

m 1Fa 2:22-24

n Met 14:29
2Ti 2:23o Met 18:6
Mhu 7:9p Met 6:10, 11
2Th 3:10

Safu ya 2

a Ayu 1:1
Lu 1:5, 6

b Zb 37:25, 26

c 1Fa 7:7

d 1Fa 3:28
Zb 72:1, 4
Met 16:12

e Ayu 14:4

f Zb 51:5
Mhu 7:20
Yak 3:2g Met 11:1
Amo 8:5
Mik 6:11

h Met 22:15

i Kut 4:11

j Met 10:4

k Met 12:11

l Law 19:13
Met 21:6

- mwa mtu ni kama maji yenye kina,
Lakini mtu mwenye uta-
mbuzi huyateka.
- 6 Watu wengi hutangaza upendo wao mshikama-nifu,
Lakini ni nani anayeweza kumpata mtu mwami-nifu?
- 7 Mwadilifu anatembea kwa utimilifu wake.^a
Watoto* wake wanaokuja baada yake watakuwa na furaha.^b
- 8 Mfalme anapoketi kwenye kiti cha ufalme ili kuhukumu,^c
Hupepetu uovu wote kwa macho yake.^d
- 9 Ni nani anayeweza kuse-
ma: "Nimeusafisha moyo wangu;^e
Mimi ni safi kutokana na dhambi yangu"?^f
- 10 Vipimo vya udanganyifu na mizani za uwongo*
—Vyote viwili humchukiza Yehova.^g
- 11 Hata mtoto* hujulikana kwa matendo yake,
Kama tabia yake ni safi na ya unyoofu.^h
- 12 Sikio linalosikia na jicho linaloona
—Yehova ameviumba vyote viwili.ⁱ
- 13 Usipende usingizi, la sivyo utakuwa maskini.^j
Fungua macho yako, nawe utashiba mkate.^k
- 14 "Si kizuri, si kizuri!" ase-
ma mnunuzi;
Kisha anaenda zake na ku-
jigamba.^l

20:7 *Tnn., "Wana." 20:10 *Au "Mawe mawili ya kupimia yaliyo tofauti na vyo-mbo viwili vya kupimia vilivyo tofauti." 20:11 *Au "mvulana."

- 15** Kuna dhahabu, pia kuna marijani* kwa wingi, Lakini midomo ya ujuzi ni kitu chenye thamani.^a
- 16** Chukua vazi la mtu ikiwa amemwekea dhamana mtu asiyemjua;^b Chukua dhamana kutoka kwake ikiwa alimfanyia hivyo mwanamke mgeni.*^c
- 17** Mkate uliopatikana kwa udanganyifu ni mtamu kwa mtu, Lakini baadaye kinywa chake kitajaa changarawe.^d
- 18** Kwa mashauriano,* mipango itafanikiwa,^e Na kwa mwelekezo stadi^Δ pigana vita vyako.^f
- 19** Mchongezi huzurura-zurura akifunua mazungumzo ya siri;^g Usishirikiane na mtu anayependa kupiga porojo.*
- 20** Yeyote anayemtukana baba yake na mama yake, Taa yake itazimwa giza litakapoingia.^h
- 21** Urithi unaopatikana kwa pupa mwanzoni Hautakuwa baraka mwi-shoni.ⁱ
- 22** Usiseme: "Nitalipiza uovu!"^j Mtumaini Yehova,^k naye atakuokoa.^l
- 23** Vipimo vya udanganyifu vinamchukiza* Yehova,

20:15 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 20:16 *Au "mgeni." 20:18 *Au "mashauri." #Au "itaimarishwa." ΔAu "mwongozo wenye hekima." 20:19 *Au "anayeshawishi kwa midomo yake." 20:23 *Au "Mawe mawili ya kupimia ya-liyo tofauti yanamchukiza."

SURA YA 20

- a Met 3:13-15
b Met 11:15
c Met 27:13
d Met 6:30, 31
e Met 15:22
f Met 11:14
Met 24:6
Lu 14:31, 32
g Law 19:16
Met 11:13
Met 25:9, 23
h Kut 20:12
Law 20:9
Met 19:26
i Met 28:8, 20
1Ti 6:9, 10
j Kum 32:35
Met 24:29
Mt 5:38, 39
Ro 12:17, 19
1Th 5:15
k Zb 37:34
l Zb 34:7
1Pe 4:19

Safu ya 2

- a Zb 37:23
Yer 10:23
b Law 27:9
c Hes 30:2
Mhu 5:4, 6
Mt 5:33
d Zb 101:8
e Isa 28:27
f Zb 61:6, 7
g Zb 21:7
h Mhu 11:9
i Law 19:32
Met 16:31
j Zb 119:71

SURA YA 21

- k Kut 14:4
Ezr 7:27
l Ne 2:7, 8
Isa 44:28
Ufu 17:17
m Zb 36:1, 2
Met 16:2
n 1Sa 16:6, 7
Met 24:12
Yer 17:10

Na mizani za uwongo si nzuri.

- 24** Hatua za mtu huongozwa na Yehova;^a Mwanadamu anawezaje kuelewa njia yake mwe-yewe?*
- 25** Ni mtego kwa mtu ku-tangaza haraka-haraka, "Ni kitakatifu!"^b Kisha anachunguza baada-ye alichoweka nadhiri.^c
- 26** Mfalme mwenye hekima huwapepetwa waovu^d Na kuwakanyaga kwa gu-rudumu la kupuria.^e
- 27** Pumzi ya mtu ni taa ya Yehova, Inayochunguza kikamili utu wake wa ndani kabisa.
- 28** Upendo mshikamanifu na uaminifu humlinda mfalme;^f Kwa upendo mshikama-nifu anadamusha kiti chake cha ufalme.^g
- 29** Utukufu wa vijana ni ngu-vu zao,^h Na fahari ya wazee ni mvi zao.ⁱ
- 30** Michubuko na majeraha huondolea mbali* uovu,^j Na mapigo husafisha utu wa ndani kabisa wa mtu.
- 21** Moyo wa mfalme ni kama vijito vya maji mkononi mwa Yehova.^k Yeye huuelekeza mahali popote anapopenda.^l
- 2** Njia zote za mwanadamu huonekana kuwa sawa machoni pake,^m Lakini Yehova huichungu-za mioyo.*ⁿ

20:24 *Au "njia ya kufuata." 20:30 *Au "husugua na kuondoa." 21:2 *Au "huzichunguza nia."

- 3** Kutenda mambo manyoo-
fu na ya haki
Humpendeza Yehova zaidi
kuliko dhabihu.^a
- 4** Macho ya kiburi na moyo
wenye majivuno
—Taa inayowaongoza wao-
vu ni dhambi.^b
- 5** Mipango ya wenye bidii
hakika huleta
mafanikio,^{*c}
Lakini wote wanaotenda
bila kufikiri kwa hakika
watakuwa maskini.^d
- 6** Kupata hazina kwa ulimi
unaosema uwongo
Ni kama ukungu unao-
toweka, mtego
unaoangamiza.^{*e}
- 7** Ukatili wa waovu utawafa-
gilia mbali,^f
Kwa maana wanakataa
kutenda haki.
- 8** Njia ya mtu mwenye hatia
imepinda,
Lakini matendo ya mtu
safi yamenyooka.^g
- 9** Ni afadhali kuishi pembe-
ni juu ya paa
Kuliko kuishi katika nyu-
mba moja na mke
mgomvi.^{*h}
- 10** Mtu mwovu hutamani
maovu;ⁱ
Hamtendei kwa fadhili
jirani yake.^j
- 11** Mwenye dhihaka ana-
poadhibiwa, asiye na
uzoefu hupata hekima
zaidi,
Na mtu mwenye hekima
anapopata ufahamu,
anapata ujuzi.^{*k}

21:5 *Au “manufaa.” 21:6 *Au labda,
“kwa wale wanaotafuta kifo.” 21:9, 19
*Au “msumbufu.” 21:11 *Au “anajua la
kufanya.”

SURA YA 21

a 1Sa 15:22, 23
Ho 6:6
Mik 6:7, 8
Mt 12:7

b Zb 10:4

c Met 13:4

d Met 14:29

e Met 1:19
Met 20:21

f Zb 7:14-16

g Zb 37:37
Met 16:17
1Pe 1:22

h Met 17:1
Met 21:19
Met 25:24
Met 27:15

i Mwa 6:5
Zb 36:1, 4

j 1Sa 25:10, 11

k Met 9:9
Met 19:25

Safu ya 2

a Mwa 19:29
Zb 37:10, 20
2Pe 2:4
2Pe 3:5, 6

b Kum 15:9
Met 28:27
Yak 5:4

c Met 18:16

d Zb 106:3

e Yak 1:15
2Pe 2:21

f Mhu 7:4
Lu 15:13, 14

g Est 7:10

h Met 17:1
Met 21:9
Met 25:24
Met 27:15

i Met 15:6
Mhu 5:19

j Lu 15:13, 14

- 12** Aliye Mwadilifu huichu-
nguza nyumba ya
mwovu;
Huwapindua waovu na ku-
waangamiza.^a
- 13** Yeyote anayeziba sikio
lake asisikie kilio cha
mtu wa hali ya chini
Yeye mwenyewe ataita
naye hatajibiwa.^b
- 14** Zawadi ya siri hutuliza ha-
sira,^c
Na rushwa iliyofichwa* hu-
tuliza ghadhabu kali.
- 15** Mwadilifu hushangilia ku-
tenda haki,^d
Lakini hilo ni jambo
baya sana kwa watenda
maovu.
- 16** Mtu anayetangatanga ku-
toka kwenye njia ya
ufahamu
Atapumzika katika kundi
la wale waliokufa ambao
hawana uwezo.^e
- 17** Anayependa raha* ataku-
wa maskini;^f
Anayependa divai na ma-
futa hatakuwa tajiri.
- 18** Mwovu ni fidia ya mwadi-
lifu,
Na mwenye hila atachuku-
liwa badala ya mnyoofu.^g
- 19** Ni afadhali kuishi nyikani
Kuliko kuishi na mke
mgomvi* anayekasirika
haraka.^h
- 20** Hazina yenye thamani na
mafuta hupatikana kati-
ka nyumba ya mwenye
hekima,ⁱ
Lakini mtu mpumbavu
atatumia vibaya* vitu
alivyo navyo.^j
- 21** Yeyote anayefuatia

21:14 *Tnn., “iliyo kifuani.” 21:17 *Au
“anasa.” 21:20 *Tnn., “atavimeza.”

- uadilifu na upendo
mshikamanifu
Atapata uzima, uadilifu,
na utukufu.^a
- 22** Mtu mwenye hekima ana-
weza kupanda katika * jiji
la watu wenye nguvu
Na kudhoofisha nguvu wa-
nazotumaini.^b
- 23** Anayelinda kinywa chake
na ulimi wake
Anajiepusha na taabu.^c
- 24** Mtu mwenye kimbelembe-
le, anayejigamba kwa
kiburi, hivyo ndivyo
unavyomwita
Mtu anayetenda kwa ki-
mbelembele bila kujali.^d
- 25** Anachotamani mtu mvivu
kitamua,
Kwa maana mikono yake
inakataa kufanya kazi.^e
- 26** Anatamani kwa pupa
mchana kutwa,
Lakini mwadilifu hutoa,
hawanyimi wengine cho-
chote.^f
- 27** Dhahibu ya mwovu ina-
chukiza.^g
Sembuse anapoitoa akiwa
na nia ovu!*
- 28** Shahidi anayesema uwo-
ngo ataangamia,^h
Lakini mtu anayesikiliza
ataoa ushahidi kwa ma-
fanikio.*
- 29** Mtu mwovu huvaa uso wa
ushupavu,ⁱ
Lakini njia ya mtu mnyoo-
fu ni hakika.*^j
- 30** Hakuna hekima, wala uta-
mbuzi wowote, wala
shauri katika kumpinga
Yehova.^k

21:22 *Au “kulishinda.” **21:27** *Au
“akiwa na mwenendo wa aibu!” **21:28**
*Tnn., “atazungumza milele.” **21:29**
*Au “mtu mnyoofu huifanya njia yake
iwe hakika.”

SURA YA 21

a Met 15:9
Met 22:4
Mt 5:6
Ro 2:6, 7

b Mhu 7:19
2Ko 10:4

c Zb 141:3
Met 10:19
Mhu 10:20

d Hes 14:44
Est 6:4

e Met 6:6-11
Met 13:4
Met 19:24

f Zb 37:25, 26
Zb 112:9
Lu 6:30

g 1Sa 15:22, 23
Met 15:8
Isa 1:11

h Kum 19:18, 19
Met 19:5

i Met 28:14
Met 29:1

j Met 11:5

k Hes 23:7, 8
Met 19:21
Mdo 5:38, 39

Safu ya 2

a Zb 20:7
Zb 33:17
Isa 31:1

b 2Nya 20:15, 17
Zb 68:20
Ufu 7:10

SURA YA 22

c Mhu 7:1

d Mdo 17:26

e Zb 34:9
Met 18:12

f Met 4:14, 15

g Mwa 18:19
Kum 6:6, 7
Efe 6:4

h 2Ti 3:14, 15

i 2Fa 4:1
Mt 18:25

j Gal 6:7, 8

k Zb 125:3

l Kum 15:7, 8
Met 11:25
Ebr 6:10

- 31** Farasi hutayarishwa kwa
ajili ya siku ya vita,^a
Lakini wokovu ni wa
Yehova.^b

22 Ni afadhali kuchagua
jina jema* kuliko mali
nyingi;^c

Kuheshimiwa[#] ni bora ku-
liko fedha na dhahabu.

- 2** Matajiri na maskini wa-
nafanana katika jambo
hili:*

Yehova aliwaumba wote.^d

- 3** Mtu mwerevu huona hata-
ri na kujificha,
Lakini wajinga husonga
mbele na kupata
madhara.*

- 4** Unyenyekevu na kumwo-
gopa Yehova huleta
Utajiri na utukufu na
uzima.^e

- 5** Miiba na mitego iko
kwenye njia ya mtu
aliyepotoka,
Lakini yeyote anayethami-
ni uhai wake* hukaa
mbali nayo.^f

- 6** Mzoeze mvulana* njia
anayapaswa kuifuata;^g
Hata atakapozeeka ha-
taiacha.^h

- 7** Tajiri humtawala maskini,
Na mkopaji ni mtumwa wa
mkopeshaji.ⁱ

- 8** Yeyote anayepanda uovu
atavuna msiba,^j
Na fimbo ya ghadhabu
yake itaangamia.^k

- 9** Mtu mkarimu* atabari-
kiwa,
Kwa maana chakula chake
humgawia maskini.^l

22:1 *Au “sifa njema.” Tnn., “jina.”
#Tnn., “Kibali.” **22:2** *Tnn., “huku-
tana.” **22:3** *Au “adhabu.” **22:5** *Au
“nafsi yake.” **22:6** *Au “mtoto; kijana.”
22:9 *Tnn., “Aliye na jicho zuri.”

- 10** Mfukuze mtu mwenye dhishaka,
Na ugomvi utatoweka;
Mizozo* na matusi yata-koma.
- 11** Mtu anayependa moyo safi
na ambaye husema ma-neno yenye fadhili
Atakuwa rafiki ya mfalme.^a
- 12** Macho ya Yehova huulinda ujuzi,
Lakini Yeye huyapindua maneno ya wenye hila.^b
- 13** Mvivu anasema: “Kuna si-mba nje!
Nitauawa katikati ya uwa-nja wa jiji!”^c
- 14** Kinywa cha wanawake waliopotoka* ni shimo refu.^d
Anayeshutumiwa na Yehova ataanguka ndani yake.
- 15** Ujinga umefungwa katika moyo wa mvulana,^{*e}
Lakini fimbo ya nidhamu ndiyo itakayouondolea mbali.^f
- 16** Anayempunja maskini ili aongeze mali yake^g
Na yule anayewapa zawadi matajiri
Mwishowe watakuwa maskini.
- 17** Tega sikio lako usikie ma-neno ya wenye hekima,^h
Ili uufanye moyo wako uzingatie ujuzi wangu,ⁱ
- 18** Kwa maana inapendeza kuyahifadhi ndani yako kabisa,^j
Ili yote yawe midomoni mwako daima.^k
- 19** Ili umtegemee Yehova,
Ninakupa ujuzi leo.

22:10 *Au “Kesi.” 22:14 *Tnn., “wage-ni.” 22:15 *Au “mtoto; kijana.”

SURA YA 22

a Zb 45:2
Met 16:13
Mt 5:8

b Mdo 13:8-10

c Met 26:13-15

d Met 5:3
Mhu 7:26

e Mwa 8:21

f Met 13:24
Met 19:18

g Zb 12:5
Met 14:31

h Met 13:20

i Met 15:14

j Met 2:10
Met 24:14

k Met 15:7

Safu ya 2

a Met 23:10

b Kut 23:6
Amo 5:12

c 1Sa 24:12
Zb 12:5

d Met 13:20

e Met 6:1-3

f Kum 19:14
Met 23:10
Ho 5:10

g 1Sa 16:18, 19
1Fa 7:13, 14

- 20** Je, tayari sijakuandikia,
Na kukupa mashauri na ujuzi,
- 21** Ili nikufundishe maneno ya kweli yanayotegemeka,
Uweze kumpelekea habari sahihi yule aliyekutuma?
- 22** Usimwibie mtu maskini kwa kuwa ni maskini,^a
Wala usimkandamize mtu wa hali ya chini katika lango la jiji.^b
- 23** Kwa maana Yehova mwenyewe atawatetea^c
Naye atawaangamiza wa-naowapunja.
- 24** Usiwe na urafiki na mtu mwenye hasira kali
Wala kushirikiana na mtu anayekasirika upesi,
- 25** Ili usijifunze kamwe njia zake
Na kujitia mtegoni.^d
- 26** Usiwe miongoni mwa wale wanaopeana mikono wa-napotoa dhamana,
Wanaoweka dhamana kwa ajili ya mikopo.^e
- 27** Ikiwa huna kitu cha kulipa,
Kitanda chako kitavutwa na kuchukuliwa ukiwa umekilalia!
- 28** Usiisogeze alama ya kale ya mpaka
Iliyowekwa na mababu zako.^f
- 29** Je, umemwona mtu aliye stadi katika kazi yake?
Atasimama mbele ya wafalme;^g
Hatasimama mbele ya watu wa kawaida.
- 23** Ukiketi kula pamoja na mfalme,
Chunguza kwa makini kilicho mbele yako;

- 2 Tia kisu kwenye koo lako*
Ikiwa una hamu kubwa ya
chakula.[#]
- 3 Usivitamani vyakula vya-
ke vitamu,
Kwa maana ni vyakula vya
udanganyifu.
- 4 Usijichoshe kupata uta-
jiri.^a
Acha, na uonyeshe uele-
waji.*
- 5 Ukiutupia jicho, haupo,^b
Kwa maana hakika utaota
mabawa kama ya tai na
kuruka mbali angani.^c
- 6 Usile chakula cha mtu
mchoyo;*
Usivitamani vyakula vyake
vitamu,
- 7 Kwa maana yeye ni kama
mtu anayeweka hesabu.*
"Kula na kunywa," ana-
kuambia, lakini sivyo
anavyoamaanisha.[#]
- 8 Utatapika matonge uliyo-
kula
Nawe utakuwa umepoteza
maneno yako ya kumsifu.
- 9 Usiongee masikioni mwa
mpumbavu,^d
Kwa maana ataidharau he-
kima ya maneno yako.^e
- 10 Usiisogeze alama ya kale
ya mpaka^f
Wala kuingia katika sha-
mba la mayatima.
- 11 Kwa maana Mtetezi* wao
ana nguvu;
Atawatetea dhidi yako.^g
- 12 Fanye moyo wako uzinga-
tie nidhamu

23:2 *Au "Jizuie." #Au "una nafsi iliyo-
jaa tamaa." 23:4 *Au labda, "Acha ku-
fuata uelewaji wako mwenyewe." 23:6
*Au "cha yeyote mwenye jicho ovu."
23:7 *Au "anayehesabu katika nafsi
yake." #Tnn., "moyo wake hauko pa-
moja nawe." 23:11 *Tnn., "Mkombozi."

SURA YA 23

a Met 28:20
Yoh 6:27
1Ti 6:9,10

b 1Yo 2:16,17

c Met 27:24

d Met 9:7
Met 26:4

e Mt 7:6

f Kum 19:14
Met 22:28

g Kut 22:22, 23
Zb 10:14

Safu ya 2

a Met 13:24
Met 19:18
Efe 6:4

b Met 27:11
3Yo 4

c Zb 37:1

d Zb 111:10
2Ko 7:1

e Zb 37:37
Met 24:14

f Met 20:1
Isa 5:11
Ro 13:13
1Pe 4:3

g Met 28:7
1Ko 10:31

h Kum 21:20, 21
Met 21:17

i Kut 20:12
Kut 21:17
Mt 15:5, 6
Efe 6:1

Na sikio lako maneno ya
ujuzi.

- 13 Usimnyime mvulana*
nidhamu.^a
Ukimpiga kwa fimbo, hata-
kufa.
- 14 Unapaswa kumpiga kwa
fimbo,
Ili umwokoee asiingie Kabu-
rini.*
- 15 Mwanangu, ikiwa moyo
wako utakuwa na
hekima,
Basi moyo wangu mimi
utashangilia.^b
- 16 Utu wangu wa ndani uta-
shangilia
Midomo yako inaposema
mambo yaliyo sawa.
- 17 Moyo wako usiwaonee
wivu watenda dhambi,^c
Bali mwogope Yehova
mchana kutwa.^d
- 18 Kwa maana ndipo utaka-
pokuwa na wakati ujao^e
Na tumaini lako halitafuti-
liwa mbali.
- 19 Mwanangu, sikiliza uwe
na hekima,
Na uuelekeze moyo wako
katika njia inayofaa.
- 20 Usiwe miongoni mwa watu
wanaokunywa divai nyi-
ngi mno,^f
Miongoni mwa wale wa-
naokula nyama kwa
pupa,^g
- 21 Kwa maana mlevi na mlafi
watakuwa maskini,^h
Na kusinzia kutamvika
mtu matambara.
- 22 Msikilize baba yako aliye-
kuzaa,
Wala usimdharau mama
yako kwa sababu tu ame-
zeeka.ⁱ

23:13 *Au "mtoto; kijana." 23:14 *Au
"Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012.

23 Inunue* kweli wala usiuze kamwe,^a

Pia hekima na nidhamu na uelewaji.^b

24 Baba ya mtu mwadilifu hakika atakuwa na shangwe;

Na baba anayemzaa mwana mwenye hekima atamfurahia.

25 Baba yako na mama yako watafurahi,

Na mama aliyekuzaa atakuwa na shangwe.

26 Mwanangu, nipe moyo wako,

Na macho yako yapendzwe na njia zangu.^c

27 Kwa maana kahaba ni shimo refu,

Na mwanamke mwasherati* ni kisima chembamba.^d

28 Hunyemelea kama mnyang'anyi;^e

Huongoza idadi ya wanau-me wasio waaminifu.

29 Ni nani mwenye ole? Ni nani aliye na wasiwasi? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani anayelalamika? Ni nani aliye na majeraha bila sababu? Ni nani aliye na macho mazito?*

30 Ni wale wanaoshinda kwenye divai;^f

Wale wanaotafuta* divai iliyochanganywa.

31 Usiitazame rangi nyekundu ya divai

Inapong'aa katika kikombe na kushuka taratibu,

SURA YA 23

a Flp 3:7, 8

b Met 4:5
Met 16:16

c Zb 107:43

d Met 22:14

e Met 7:10, 12
Mhu 7:26

f Met 20:1
Efe 5:18

Safu ya 2

a Ho 4:11

b Mwa 19:33

SURA YA 24

c Zb 26:5
Met 1:10

d Met 9:1
Met 14:1

e 1Fa 10:23
Met 15:6

f Met 8:14
Met 21:22

g Met 20:18
Lu 14:31, 32

32 Kwa maana mwishowe huuma kama nyoka, Nayo hutoa sumu kama nyoka kipiri.

33 Macho yako yataona mambo ya ajabu, Na moyo wako utasema mambo yaliyopotoka.^a

34 Nawe utakuwa kama mtu anayelala katikati ya bahari,

Kama mtu anayelala juu ya mlingoti wa meli.

35 Utasema: "Wamenipiga, lakini sikuhihi chochote.*

Waliniipiga, lakini sikujua. Nitaamka lini?^b

Nahitaji kinywaji kingine."[#]

24 Usiwaonee wivu waovu, Wala usitamani kushirikiana nao,^c

2 Kwa maana moyo wao hutafakari ukatili, Na midomo yao huongea kuhusu kuwataabisha wengine.

3 Nyumba* hujengwa kwa hekima,^d

Na kwa utambuzi hufanywa iwe salama.

4 Kwa ujuzi vyumba hujazwa

Kila aina ya hazina zenye thamani na zinazopendeza.^e

5 Mtu mwenye hekima ana nguvu,^f

Na kwa ujuzi mtu huzidisha nguvu zake.

6 Kwa mwelekezo stadi* utapigana vita vyako,^g

23:23 *Au "Jipatie." 23:27 *Tnn., "mgeni." Angalia Met 2:16. 23:29 *Au "macho yaliyochoka." 23:30 *Au "wanaokusanyika ili kuonjaonja."

23:35 *Au "sikuhihi uchungu." #Au "Nitaitafuta divai tena." 24:3 *Au "Familia." 24:6 *Au "mwongozo wenye hekima."

- Na kupitia washauri wengi kuna ushindi.*^a
- 7** Mjinga hawezi kupata hekima ya kweli;^b
Hana lolote la kusema katika lango la jiji.
- 8** Yeyote anayepanga njama ya uovu
Ataitwa stadi wa kupanga hila.^c
- 9** Njama za upumbavu* ni dhambi,
Na watu humchukia mwenye dhihaka.^d
- 10** Ukivunjika moyo siku ya taabu,*
Nguvu zako zitakuwa chache.
- 11** Waokoe wale wanaopeleka kwenye kifo,
Na uwazuie wale wanaopepesuka wakieleka kuchinjwa.^e
- 12** Ukisema: "Lakini hatukujua jambo hili,"
Je, Yule anayeichunguza moyo* hatatambua hilo?^f
Naam, Yule anayekutazama atajua
Naye atamlipa kila mwanadamu kulingana na matendo yake.^g
- 13** Mwanangu, kula asali, kwa sababu ni njema;
Asali ya sega ni tamu kinnywani.
- 14** Vivyo hivyo, jua kwamba hekima ina manufaa kwako.*^h
Ukiipata, utakuwa na wakati ujao

24:6 *Au "wokovu." 24:9 *Au "Njama za mpumbavu." 24:10 *Au "nyakati za taabu." 24:12 *Au "anayechunguza nia." 24:14 *Au "ni tamu kwa nafsi yako."

SURA YA 24

a Met 11:14
Met 13:10
Met 15:22
Mdo 15:5, 6

b Met 14:6
IKo 2:14

c Met 6:12-14

d Met 22:10

e Zb 82:4

f Met 5:21
Met 17:3
Met 21:2

g Zb 62:12
Mt 16:27
Ro 2:5, 6

h Zb 19:9, 10
Zb 119:103

Safu ya 2

a Met 23:18

b Zb 34:19
2Ko 1:10

c 1Sa 26:9, 10
Est 7:10

d Ayu 31:29
Met 17:5
Met 25:21, 22

e Eze 26:2, 3
Zek 1:15

f Zb 73:18, 27
Met 10:7

g Met 13:9

h 1Sa 24:6, 7
1Pe 2:17

i 2Sa 15:12

j Hes 16:2, 31

k Met 20:2

Na tumaini lako halitafuti-liwa mbali.^a

- 15** Usivizie kwa uovu karibu na makao ya mtu mwadilifu;
Usiharibu mahali pake pa kupumzikia.
- 16** Kwa maana mwadilifu anaweza kuanguka mara saba, lakini atainuka tena,^b
Lakini waovu watakwazwa na msiba.^c
- 17** Adui yako akianguka, usishangilie,
Na akijikwaa, usiruhusu moyo wako uwe na shangwe;^d
- 18** La sivyo, Yehova ataona jambo hilo naye hatafuraahi,
Naye ataiondoa hasira yake kumweleka.*^e
- 19** Usifadhaike* kwa sababu ya waovu;
Usiwaonee wivu watu waovu,
- 20** Kwa maana mtu yeyote mwovu hana wakati ujao;^f
Taa ya waovu itazimwa.^g
- 21** Mwanangu, mwogope Yehova na mfalme.^h
Nawe usishirikiane na waasi,*ⁱ
- 22** Kwa maana msiba wao utatokea ghafla.^j
Ni nani anayejua jinsi wote wawili* watakavyowaa-ngamiza?^k
- 23** Haya pia ni maneno ya wenyewe hekima:
Kuonyesha upendeleo

24:18 *Yaani, yule adui. 24:19 *Au "Usiwake hasira." 24:21 *Au "wale wanaotaka mabadiliko." 24:22 *Yaani, Yehova na mfalme.

katika hukumu si jambo zuri.^a

- 24** Yeyote anayemwambia mtu mwovu, "Wewe ni mwadilifu,"^b
Atalaaniwa na watu na ku-shutumiwa na mataifa.
- 25** Lakini mambo yatawae-ndea vema wale wanaomkaripia;^c
Watapata baraka ya vitu vyema.^d
- 26** Watu wataibusu midomo ya mtu anayejibu kwa unyoofu.^{*e}
- 27** Tayarisha kazi yako ya nje, na utayarishe kila kitu shambani;
Kisha uijenge nyumba* yako.
- 28** Usitoe ushahidi dhidi ya jirani yako pasipo msi-ngi.^f
Usiitumie midomo yako kuwadanganya wengine.^g
- 29** Usiseme: "Nitamtendea kama tu alivyonitendea; Nitamlipiza kwa sababu ya mambo aliyonitendea."^{*h}
- 30** Nilipita karibu na shamba la mtu mvivu,ⁱ
Karibu na shamba la mi-zabibu la mtu asiye na busara.*
- 31** Niliona limejaa magugu; Ardhi ilifunikwa na miiba, Na ukuta wake wa mawe ulikuwa umebomoka.^j
- 32** Nilitazama hilo na kulitia moyoni;
Nililiona na kujifunza somo hili:*
- 33** Lala kidogo, sinzia kidogo,

24:26 *Au labda, "Kujibu kwa unyoofu ni kama kumbusu mtu." **24:27** *Au "familia." **24:29** *Au "Nitamlipa sawasawa na matendo yake." **24:30** *Tnn., "aliyepungukiwa moyoni." **24:32** *Tnn., "Nilipokea nidhamu."

SURA YA 24

a Law 19:15
Kum 1:16, 17
Kum 16:19
2Nya 19:7
1Ti 5:21

b Met 17:15

c Law 19:17
1Ti 5:20

d Met 28:23

e Met 27:5

f Kut 20:16

g Efe 4:25

h Met 20:22
Ro 12:17, 19
1Th 5:15

i Met 6:10, 11

j Met 20:4
Met 22:13
Mhu 10:18

Safu ya 2

a Met 10:4
Met 23:21

SURA YA 25

b 1Fa 4:29, 32
Mhu 12:9

c 2Nya 29:1

d Kum 29:29
Ro 11:33

e Met 17:3

f 1Fa 2:44, 46
Met 20:28
Met 29:14

g Met 27:2

h Zb 131:1

i Lu 14:8-10
1Pe 5:5

j Met 18:17
Mt 5:25

k Mt 18:15

Kunja mikono kidogo ili upumzike,

- 34** Na umaskini wako utakuja kama jambazi,
Na uhitaji wako kama mwanamume mwenye silaha.^a

25 Hizi pia ni methali za Sulemani^b zilizopakiliwa* na watu wa Hezekia^c mfalme wa Yuda:

- 2** Ni utukufu wa Mungu kutunza jambo likiwa siri,^d
Na utukufu wa wafalme ni kulichunguza jambo kabisa.

- 3** Kama mbingu zilivyo juu na kama dunia ilivyo na kina,
Ndivyo moyo wa wafalme usivyochunguzika.

- 4** Ondoa takataka katika fedha,
Nayo itakuwa safi kabisa.^e

- 5** Mwendoe mtu mwovu mbele ya mfalme,
Na kiti chake cha ufalme kitaimarishwa kabisa katika uadilifu.^f

- 6** Usijiheshimu mwenyewe mbele ya mfalme,^g

Wala usijiingize miongoni mwa watu mashuhuri,^h

- 7** Kwa maana ni afadhali yeye akuambie, "Njoo hapa juu,"
Kuliko akuambishe mbele ya mkuu.ⁱ

- 8** Usiharakishe kupeleka kesi mahakamani,
Kwa maana utafanya nini baadaye jirani yako aki-kuaibisha?^j

- 9** Suluhisha jambo hilo na jirani yako,^k

25:1 *Au "zilizopakiliwa na kukusanywa."

- Lakini usifunue uliyoambiwa sirini,*^a
- 10** Ili anayesikiliza asikuai-bishe
Nawe ueneze habari mba-ya ambayo haiwezi* kubatilishwa.
- 11** Kama matofaa ya dhahabu yalinyakshiwa kwenye vyombo vya fedha
Ndivyo lilivyo neno linalo-semwa wakati unaofaa.^b
- 12** Kama kipuli cha dhahabu na pambo la dhahabu bora
Ndivyo alivyo mkaripiaji mwenye hekima kwa sikio linalosikia.^c
- 13** Kama baridi ya theluji siku ya mavuno
Ndivyo alivyo mjumbe mwaminifu kwa wale wa-naomtuma,
Kwa maana yeye humburudisha bwana wake.^d
- 14** Kama mawingu na upepo usioleta mvua
Ndivyo alivyo mtu anayejigamba kwamba atatoa zawadi lakini haitoi kamwe.*^e
- 15** Kwa subira kamanda hushawishiwa,
Na ulimi laini* unaweza kuvunja mfupa.^f
- 16** Ukipata asali, kula kiasi kinachokutosha,
Kwa maana ukiila kupita kiasi, huenda ukaita-pika.^g
- 17** Mguu wako na uwe haba katika nyumba ya jirani yako,
Ili asikuchoke na kukuchukia.

25:9 *Au "usifunue siri za wengine."
25:10 *Au "uvumi unaodhuru ambao hauwezi." 25:14 *Tnn., "kuhusu zawadi ya uwongo." 25:15 *Au "mpole."

SURA YA 25

a Met 11:13

b Met 15:23
Isa 50:4c Zb 141:5
Met 1:8,9
Met 9:8

d Met 13:17

e Mt 5:37

f Mwa 32:4, 5
Met 15:1

g Met 25:27

Safu ya 2

a Kut 20:16

b Zb 137:3, 4

c Kut 23:5
2Fa 6:21, 22
Met 24:17
Mt 5:44

d Ro 12:20

e Zb 101:5

f Met 21:9,19
Met 27:15g Met 15:30
Isa 52:7

- 18** Kama rungu la vita na upanga na mshale mkali
Ndivyo alivyo mtu anayetoa ushahidi wa uwongo dhidi ya jirani yake.^a
- 19** Kama jino lililovunjika au mguu unaochechemea
Ndivyo ilivyo kumtumaini mtu asiyetegemeka* nyakati za taabu.
- 20** Kama mtu anayevua nguo siku ya baridi
Na kama siki iliyomwagwa kwenye magadi
Ndivyo alivyo mtu anayeuimbua nyimbo moyo wenye huzuni.^b
- 21** Ikiwa adui yako* ana njaa, mpe mkate ale;
Ikiwa ana kiu, mpe maji anywe.^c
- 22** Kwa maana utakuwa unakusanya makaa ya mawe yanayowaka juu ya kichwa chake,*^d
Na Yehova atakuthawabi-sha.
- 23** Upepo wa kaskazini huleta mvua,
Na ulimi unaopiga porojo huleta uso wenye hasira.^e
- 24** Ni afadhali kuishi pembeni juu ya paa
Kuliko kuishi katika nyumba moja na mke mgomvi.*^f
- 25** Kama maji baridi kwa nafsi* iliyochoka
Ndivyo ilivyo habari njema kutoka nchi ya mbali.^g
- 26** Kama chemchemi yenye
- 25:19 *Au labda, "mtu mwenye hila."
25:21 *Tnn., "anayekuchukia." 25:22 *Yaani, kupunguza uadui wake na kuyeyusha ugumu wake. 25:24 *Au "msumbufu." 25:25 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

matope na kisima kili-
chochafuliwa

Ndivyo alivyo mtu mwa-
dilifu anayekubali
kumfuata* mtu mwovu.

27 Si viziri kula asali nyingi
mno,^a

Wala si utukufu kujitafutia
utukufu wako mwe-
nyewe.^b

28 Kama jiji lililobomolewa,
lisilo na ukuta,
Ndivyo alivyo mtu asi-
yeweza kuidhibiti hasira
yake.*^c

26 Kama theluji wakati wa
kiangazi na mvua wa-
kati wa mavuno,
Ndivyo heshima isivyo-
mfaa mpumbavu.^d

2 Kama ndege alivyo na sa-
babu ya kukimbia na
mbayuwayu kuruka,
Ndivyo laana isivyokuja
bila sababu nzuri.*

3 Mjeledi ni wa farasi, lija-
mu ni ya punda,^e
Na fimbo ni ya mgongo wa
watu wapumbavu.^f

4 Usimjibu mpumbavu kuli-
ngana na ujinga wake,
Ili usiwe kama yeye.*

5 Mjibu mpumbavu kulinga-
na na ujinga wake,
Ili asifikiri kwamba ana
hekima.^g

6 Kama mtu anayeilemaza
miguu yake na kujidhuru
mwenyewe*
Ndivyo alivyo mtu ana-
yemkabidhi mambo
mpumbavu.

25:26 *Au "anayekubaliana na." Tnn.,
"anayepesuka mbele ya." 25:28 *Au
"asiyeweza kuizua roho yake." 26:2
*Au labda, "Ndivyo laana isiyostahiliwa
isivyompata mtu." 26:4 *Au "Ili usili-
ngane naye." 26:6 *Tnn., "kunywa uka-
titi."

SURA YA 25

a Met 25:16

b Met 27:2
Yoh 5:44
Flp 2:3

c 1Sa 20:33
Met 16:32
Met 22:24, 25
Met 29:11

SURA YA 26

d Met 30:21, 22
Mhu 10:7

e Zb 32:9

f Met 27:22

g Mt 21:23-25

Safu ya 2

a Met 17:7

b Met 19:10
Met 26:1

c 2Pe 2:22

d Met 12:15
1Ko 3:18
1Ko 8:2

e Met 22:13

f Met 6:9
Met 19:15
Met 24:33, 34

g Met 19:24

7 Kama miguu inayocheche-
mea* ya walemavu,
Ndivyo ilivyo methali
kinywani mwa watu wa-
pumbavu.^a

8 Kama jiwe linavyofungwa
kwenye kombeo,
Ndivyo ilivyo kumpa utu-
kufu mtu mpumbavu.^b

9 Kama mmea wa miiba
mkononi mwa mlevi,
Ndivyo ilivyo methali
kinywani mwa watu wa-
pumbavu.

10 Kama mpiga mishale ana-
yemjeruhi yeyote yule,*
Ndivyo alivyo mtu ana-
yemwajiri mpumbavu au
wapita njia.

11 Kama mbwa anayerudia
matapishi yake,
Ndivyo mpumbavu ana-
vyorudia ujinga wake.^c

12 Je, umemwona mtu anaye-
fikiri ana hekima?^d
Kuna tumaini zaidi kwa
mpumbavu kuliko kwa
mtu huyo.

13 Mvivu anasema: "Kuna
mwanasimba baraba-
rani,
Kuna simba katika uwanja
wa jiji!"^e

14 Mlango huzunguka-
zunguka katika bawaba
zake,*
Na mvivu hugeuka-geuka
kitandani mwake.^f

15 Mvivu huutumbukiza*
mkono wake katika ba-
kuli la karamu,
Lakini amechoka sana
kuurudisha kinywani
mwake.^g

26:7 *Au "inayoning'inia." 26:10 *Au
"anayemjeruhi kila mtu." 26:14 *Au
"maegemeo yake." 26:15 *Tnn., "huu-
zika."

- 16** Mvivu hufikiri kwamba ana hekima zaidi
Kuliko watu saba wanaoji-
bu kwa busara.
- 17** Kama mtu anayemkamata mbwa masikio
Ndivyo alivyo mpita
njia anayekasirishwa na*
ugomvi usiomhusu.^a
- 18** Kama mwenda wazimu anayetupa vishale vina-
vyowaka moto, mishale,
na kifo*^c
- 19** Ndivyo alivyo mtu anaye-
mhadaa jirani yake na
kusema, “Nilikuwa niki-
fanya mzaha tu!”^b
- 20** Pasipo na kuni moto huzi-
mika,
Na pasipo na mchongezi,
ugomvi hukoma.^c
- 21** Kama makaa yanavyoo-
ngezwa kwenye makaa
yanayozimika na kuni zi-
navyoongezwa motoni,
Ndivyo mtu mgomvi ana-
vyochocha ugomvi.^d
- 22** Maneno ya mchongezi ni
kama matonge matamu;*
Humezwa na kushuka tu-
mboni moja kwa moja.^e
- 23** Kama fedha inayopakwa
juu ya chombo cha
udongo
Ndivyo yalivyo maneno ya
upendo yanayotoka kati-
ka* moyo mwovu.^f
- 24** Anayewachukia wengine
huficha chuki hiyo kwa
midomo yake,
Lakini ndani amesitiri
udanganyifu.
- 25** Ingawa anaongea kwa fa-
dhili, usimwamini,

26:17 *Au labda, “anayekiingiza katika.”
26:18 *Au “mishale inayoua.” 26:22
*Au “vitu vinavyomezwa kwa pupa.”
26:23 *Tnn., “Ndivyo ilivyo midomo ye-
nye shauku pamoja na.”

SURA YA 26

a 1Th 4:11
1Pe 4:15

b Met 15:21

c Met 22:10
Yak 3:6

d Met 3:30
Met 16:28
Met 17:14

e Met 18:8

f 2Sa 20:9,10

Safu ya 2

a Est 7:10
Zb 9:15
Met 28:10
Mhu 10:8

b Met 29:5

SURA YA 27

c Lu 12:19, 20
Yak 4:13,14

d Met 25:27
Yer 9:23
2Ko 10:18

e 1Sa 25:25

f Mwa 37:9-11
Met 14:30
Mdo 17:5

g Law 19:17
Mt 18:15

h 2Sa 12:7,9
Zb 141:5
Ufu 3:19

Kwa maana kuna mambo
saba yanayochukiza mo-
yoni mwake.*

- 26** Ingawa chuki yake imefi-
chwa kwa udanganyifu,
Uovu wake utafunuliwa
kutanikoni.
- 27** Anayechimba shimo ataa-
nguka ndani yake,
Na yeyote anayebingirisha
jiwe—litamrudia.^a
- 28** Ulimi unaosema uwongo
huwachukia watu ulio-
waponda,
Na kinywa kinachosifusifu
huleta uharibifu.^b

27 Usijigambe kuhusu
kesho,

Kwa maana hujui siku ita-
leta nini.*^c

- 2** Acha mtu mwingine* aku-
sifu, wala si kinywa
chako mwenyewe;
Wengine,[#] wala si midomo
yako mwenyewe.^d
- 3** Jiwe ni zito na mchanga ni
mzito sana,
Lakini usumbufu unaosa-
babishwa na mjinga ni
mzito kuliko vyote
viwili.^e
- 4** Kuna ukatili wa ghadhabu
na mafuriko ya hasira,
Lakini ni nani anayeweza
kustahimili wivu?^f
- 5** Karipio la wazi ni afadhali
kuliko upendo uliofi-
chwa.^g
- 6** Majeraha yanayosababi-
shwa na rafiki ni ya
uaminifu,^h
Lakini mabusu ya adui ni
mengi.*

26:25 *Au “Kwa maana moyo wake una-
chukiza kabisa.” 27:1 *Tnn., “itazaa
nini.” 27:2 *Tnn., “mtu asiyekujua.”
#Tnn., “Wageni.” 27:6 *Au labda, “si
ya unyoofu; ni ya kulazimishwa.”

- 7** Yule aliyetosheleza hamu yake hukataa* asali ya sega,
Lakini kwa mwenye njaa, hata kilicho kichungu ni kitamu.
- 8** Kama ndege anayeenda* mbali kutoka kwenye kiota chake
Ndivyo alivyo mtu anayetangatanga mbali kutoka nyumbani kwake.
- 9** Mafuta na uvumba huufanya moyo ushangilie;
Ndivyo ulivyo urafiki mtamu unaochipuka kutokana na shauri la unyoofu.*^a
- 10** Usimwache rafiki yako au rafiki ya baba yako,
Wala usiingie katika nyumba ya ndugu yako siku ya msiba wako;
Ni afadhali jirani aliye karibu kuliko ndugu aliye mbali.^b
- 11** Uwe na hekima, mwanaangu, na kuufanya moyo wangu ushangilie,^c
Ili niweze kumjibu yule anayenidhihakia.^d
- 12** Mtu mwerevu huona hataari na kujificha,^e
Lakini wajinga husonga mbele na kupata madhara.*
- 13** Chukua vazi la mtu ikiwa amemdhamini mtu asiye mjua;
Chukua dhamana kutoka kwake ikiwa alimfanyia hivyo mwanamke mgeni.*^f
- 14** Mtu akimbariki jirani yake

27:7 *Tnn., "huikanyagia chini." 27:8 *Au "anayekimbia." 27:9 *Au "shauri la nafsi." 27:12 *Au "adhabu." 27:13 *Au "mgeni."

SURA YA 27

a 1Sa 23:16
Met 15:23
Met 16:24

b Met 17:17
Met 18:24

c Met 10:1
Met 23:15
2Yo 4

d Ayu 1:8, 9

e Met 18:10
Isa 26:20
Ebr 11:7

f Met 20:16

Safu ya 2

a Met 21:9, 19

b 1Sa 23:16
Ebr 10:24, 25

c Met 13:4

d Mwa 39:2
Met 17:2

e Met 30:15, 16

f Met 17:3

kwa sauti kubwa asubuhi na mapema,
Itaonwa kuwa laana.

- 15** Mke mgomvi* ni kama paa linalovuja maji mfululizo siku ya mvua.^a
- 16** Yeyote anayeweza kumzuia anaweza kuuzuia upepo
Naye anaweza kuyakamata mafuta kwa mkono wake wa kulia.
- 17** Kama chuma kinavyonoa chuma,
Ndivyo mtu anavyomnoa* rafiki yake.^b
- 18** Anayeitunza mtini atakula matunda yake,^c
Na anayemtunza bwana wake ataheshimiwa.^d
- 19** Kama maji yanavyoonyesha* uso wa mtu,
Ndivyo moyo wa mtu unavyoonyesha* moyo wa mwingine.
- 20** Kaburi na mahali pa maa ngamizi* havitosheki kamwe,^e
Wala macho ya mwanadamu hayatosheki kamwe.
- 21** Chungu cha kusafishia ni kwa ajili ya fedha na tanuru ni kwa ajili ya dhahabu,^f
Vivyo hivyo mtu hupimwa kwa sifa anayopokea.*
- 22** Hata ukimtwanga mpumwavu kwa mchi*
Kama nafaka iliyoondwa katika kinu,
Upumbavu wake hautamtoka.

27:15 *Au "msumbufu." 27:17 *Tnn., "anavyoonya uso wa." 27:19 *Au "yanavyoakisi." #Au "unavyoakisi." 27:20 *Au "Sheoli na Abadoni." 27:21 *Au "Vivyo hivyo mtu hulingana na sifa yake." 27:22 *Au "mtwangio."

23 Unapaswa kujua vizuri hali ya kundi lako.

Watunze vizuri* kondoo wako,^a

24 Kwa maana mali haidumu milele,^b

Wala taji halidumu vizazi vyote.

25 Majani mabichi hutoweka, na majani mapya huchipuka,

Na majani ya milimani yanakusanywa.

26 Wanakondoo dume hukupatia mavazi yako, Na mbuzi dume hukupatia malipo ya shamba.

27 Nawe utakuwa na maziwa ya mbuzi yanayotosha kukulisha wewe, Kulisha familia yako, na kuwategemeza vijakazi wako.

28 Waovu hukimbia ingawa hakuna yeyote anayewakimbiza,

Lakini waadilifu wana ujasiri kama simba.*^c

2 Kunapokuwa na uovu* nchini, nchi inakuwa na kiongozi mmoja baada ya mwingine,^d

Lakini kwa msaada wa mtu mwenye utambuzi na ujuzi, kiongozi atadumu kwa muda mrefu.^e

3 Mtu maskini anayempunja mtu wa hali ya chini^f Ni kama mvua inayofagilia mbali chakula chote.

4 Wale wanaoiacha sheria humsifu mtu mwovu, Lakini wale wanaoishika sheria huwakasirikia.^g

27:23 *Au "Uweke moyo kwa; Wakazie uangalifu." 28:1 *Au "mwanasimba."

28:2 *Au "uasi."

SURA YA 27

a Kol 3:23

b Met 23:4, 5
1Ti 6:17

SURA YA 28

c Da 3:16, 17
Mdo 4:13

d 1Fa 16:8, 15
1Fa 16:22

e Da 4:27

f Met 14:31

g Hes 25:6-8
1Sa 15:22, 23
Efe 5:11

Safu ya 2

a Zb 25:14
Mk 4:11, 12
Yak 1:5

b Met 16:8
Met 19:1

c Met 23:20
1Ko 15:33

d Kum 23:19

e Met 13:22
Met 19:17

f Zb 66:18
Met 15:29
Isa 1:15

g Zb 7:14-16

h Kum 7:12
Zb 37:11, 18
Zb 84:11

i Met 18:11

j Mk 10:21

k 1Fa 17:1-3
Met 29:2

l 1Sa 15:13-15

m 2Sa 12:13
2Nya 33:12, 13
Zb 32:3, 5
Zb 5:1

5 Waovu hawawezi kuelewa haki,

Lakini wale wanaomtafuta Yehova wanaweza kuelewa mambo yote.^a

6 Ni afadhali maskini anayetembea kwa utimilifu wake

Kuliko tajiri ambaye njia zake zimepotoka.^b

7 Mwana mwenye uelewaji hushika sheria,

Lakini rafiki ya walafi humwaibisha baba yake.^c

8 Anayezidisha mali zake kwa faida^d na riba Humkusanyia yule anayemtendea maskini kwa fadhili.^e

9 Anayekataa kusikiliza sheria

—Hata sala yake inachukiza.^f

10 Anayempotosha mnyoofu afuate njia ya uovu atanguka katika shimo lake mwenyewe,^g

Lakini wasio na lawama watarithi kilicho chema.^h

11 Tajiri hujiona mwenyewe kuwa mwenye hekima,ⁱ Lakini mtu maskini aliye na utambuzi anaweza kumchunguza kabisa.^j

12 Waadilifu wanaposhinda, kuna utukufu mwingi, Lakini waovu wanapopata mamlaka, watu huji-ficha.^k

13 Anayefunika makosa yake hatafanikiwa,^l

Lakini yeyote anaye-yaungama na kuyaacha ataonyeshwa rehema.^m

14 Mwenye furaha ni mtu aliye chonjo sikuzote,ⁿ

28:14 *Au "anayeogopa nyakati zote."

Lakini yeyote anayeufanya moyo wake kuwa mgumu ataanguka katika msiba.^a

15 Kama simba anayenguruma na dubu anayeshambulia

Ndivyo alivyo mtawala mwovu anayewatawala watu wasio na uwezo.^b

16 Kiongozi asiye na utambuzi hutumia vibaya mamlaka yake,^c

Lakini mtu anayechukia faida isiyo ya haki atarefusha maisha yake.^d

17 Mtu aliyelemewa na hatia ya damu kwa sababu ya kumuua mwingine* atandelea kukimbia mpaka kaburini.^{#e}

Mtu yeyote asimsaidie.

18 Anayetembea bila kosa ataokolewa,^f

Lakini yule ambaye njia zake zimepotoka ataananguka ghafla.^g

19 Anayelima ardhi yake atakuwa na chakula kingi,*

Lakini anayefuatia vitu visivyo na thamani atakuwa na umaskini wa kutosha.^h

20 Mtu mwaminifu atapata baraka nyingi,ⁱ

Lakini anayeharakisha kupata utajiri hatabaki bila hatia.^j

21 Si vema kuonyesha upe ndeleo;^k

Lakini mtu anaweza kukosea kwa sababu ya kipande cha mkate.

22 Mtu mwenye wivu* hujitahidi sana kupata mali,

28:17 *Au "aliyelemewa na damu ya nafsi." #Au "shimoni." **28:19** *Tnn., "mkate mwingi." **28:22** *Au "pupa."

SURA YA 28

a Kut 7:22
Ne 9:29
Met 29:1
Yer 16:12, 13

b Sef 3:3
Mt 2:16

c Ne 5:15
Amo 4:1

d Isa 33:15, 16

e Mwa 9:6
1Fa 21:19
Mt 27:3-5

f Zb 25:21

g Zb 73:12, 18
1Th 5:3
Ufu 3:3

h Met 23:21
Lu 15:13, 14

i 1Sa 18:5
Ne 7:2
Zb 101:6

j 2Fa 5:20-22
Yer 17:11
1Ti 6:9

k Law 19:15
Met 18:5
Yak 2:1

Safu ya 2

a 2Sa 12:7, 9
Gal 2:11

b Zb 141:5
Met 27:6

c Mk 7:10, 11

d Met 19:26

e 1Fa 3:11-13

f Met 3:5
Yer 17:9

g Ayu 28:28

h Kum 15:7, 10
Zb 41:1
Met 19:17
Ebr 13:16

i Est 8:17

SURA YA 29

j Kut 11:10
2Nya 36:11-13

k 1Sa 2:22-25
2Nya 36:15, 16

l Est 3:13, 15

m Met 27:11

Lakini hajui kwamba umaskini utamkumba.

23 Yeyote anayemkaripia mwingine^a hatimaye atapata kibali zaidi^b

Kuliko mtu anayesifusifu kwa ulimi wake.

24 Yeyote anayemwibia baba yake na mama yake na kusema, "Si kosa,"^c

Ni rafiki ya mtu anayesababisha uharibifu.^d

25 Mtu mwenye pupa* huchochea mgawanyiko, Lakini yeyote anayemtegemea Yehova atapata ufanisi.^{#e}

26 Yeyote anayeutumaini moyo wake mwenyewe ni mpumbavu,^f

Lakini anayetembea kwa hekima ataponyoka.^g

27 Yeyote anayewapa maskini hatakosa chochote,^h

Lakini yule anayewafumbia macho atapata laana nyingi.

28 Waovu wanapopata mamlaka, mtu hujificha, Lakini wanapoangamia, waadilifu huongezeka.ⁱ

29 Mtu anayeifanya shingo yake kuwa ngumu baada ya kukaripiwa sana/^j

Atavunjwa kwa ghafla, naye hataweza kupona.^k

2 Waadilifu wanapokuwa wengi, watu hushangilia, Lakini mwovu anapotawala, watu hulia kwa maumivu.^l

3 Mtu anayependa hekima humfanya baba yake ahangilie,^m

28:25 *Au labda, "Nafsi yenye kiburi." #Tnn., "atanenepesha."

Lakini rafiki ya makahaba hutumia vibaya mali yake.^a

- 4** Kwa haki mfalme huleta uthabiti nchini,^b Lakini mtu anayetafuta rushwa huiharibu.
- 5** Mtu anayemsifusifu jirani yake Anautandaza wavu wa kuitana miguu yake.^c
- 6** Kosa la mtu mbaya humnasa yeye mwenyewe,^d Lakini mwadilifu hupaza sauti kwa shangwe na kufurahi.^e
- 7** Mwadilifu hujali haki za kisheria za maskini,^f Lakini mwovu hajali kamwe.^g
- 8** Watu wanaojigamba huuwasha moto mji,^h Lakini wenye hekima hutuliza hasira.ⁱ
- 9** Mtu mwenye hekima anapobishana na mpumbavu, Kutakuwa na kelele na dhihaka, lakini hawatari dhika.^j
- 10** Watu wenye kiu ya damu humchukia mtu yeyote asiye na hatia,^{*k} Nao hujaribu kumuua mnyoofu.[†]
- 11** Mtu mpumbavu humwaga hisia zake zote,^{*l} Lakini mwenye hekima huzizuia kwa utulivu.^m
- 12** Mtawala anaposikiliza uwongo, Watumishi wake wote watakuwa waovu.ⁿ
- 13** Maskini na mkandamizaji

29:10 *Au "lawama." †Au labda, "Lakini mnyoofu hujaribu kuulinda uhai wake." 29:11 *Tnn., "roho yake yote."

SURA YA 29

a Met 5:8-10
Met 6:26
Lu 15:13,14

b 2Sa 8:15
Zb 89:14
Isa 9:7

c Met 26:28
Ro 16:18

d Met 5:22

e Zb 97:11

f Zb 41:1

g Yer 5:28

h Yak 3:6

i Mdo 19:29, 35

j Met 26:4

k Mwa 27:41
1Sa 20:31
1Yo 3:11, 12

l Met 12:16
Met 25:28

m Met 14:29

n 1Fa 21:8-11
Yer 38:4, 5

Safu ya 2

a Zb 72:1, 2

b Met 20:28
Met 25:5
Isa 9:7

c Met 22:6
Met 22:15
Met 23:13
Efe 6:4

d Zb 37:34
Ufu 18:20

e Ebr 12:11

f Ho 4:6

g Met 19:16
Yoh 13:17
Yak 1:25

h Met 26:3

i Mhu 5:2
Yak 1:19

j Met 14:29
Met 21:5

k Met 15:18

l 1Sa 18:8, 9
Yak 3:16

wanafanana katika jambo hili.*

Yehova huyapa nuru macho ya wote wawili.[†]

- 14** Mfalme anapowahukumu maskini kwa haki,^a Kiti chake cha ufalme kitakuwa salama daima.^b
- 15** Fimbo* na karipio hufunza hekima,^c Lakini mtoto aliyeachiliwa humwaibisha mama yake.
- 16** Waovu wanapongezeka, uovu huongezeka, Lakini waadilifu watawona wakianguka.^d
- 17** Mtie nidhamu mwana wako naye atakupumzisha; Atakufurahisha sana.^e
- 18** Wakati hakuna maono,* watu hufanya wape ndavyo,^f Lakini wenye furaha ni wale wanaoishika sheria.^g
- 19** Mtumishi hata kubali kurekebisha kwa maneno, Kwa maana ingawa anaelewa, hatii.^h
- 20** Je, umemwona mtu anayeongea bila kufikiri?ⁱ Kuna tumaini zaidi kwa mjinga kuliko yeye.^j
- 21** Mtumishi akibembelezwa tangu ujana wake, Baadaye atakuwa mtu asiye na shukrani.
- 22** Mtu anayekasirika upesi huchochea ugomvi;^k Yeyote aliye mwepesi wa ghadhabu hufanya makosa mengi.^l

29:13 *Tnn., "hukutana pamoja." †Yaani, Huwapa uhai. 29:15 *Au "Nidhamu; Adhabu." 29:18 *Au "maono ya kinabii; ufunuo."

23 Kiburi cha mtu kitamnye-
nyekeza,^a

Lakini yeyote aliye mnye-
nyekevu rohoni atapata
utukufu.^b

24 Rafiki ya mwizi hujichukia
mwenyewe.

Huenda akasikia tangazo
la kutoa ushahidi, * laki-
ni hatoi habari yoyote.^c

25 Kuwaogopa* wanadamu ni
mtego,^d

Lakini yule anayemtumai-
ni Yehova atalindwa.^e

26 Watu wengi hutaka kuku-
tana na* mfalme,

Lakini mtu hupata haki
kutoka kwa Yehova.^f

27 Mtu asiyetenda haki hu-
mchukiza mwadilifu,^g

Lakini yule ambaye njia
yake imenyooka hu-
mchukiza mwovu.^h

30 Ujumbe mzito wa Agu-
ri mwana wa Yake, alio-
mwambia Ithieli, naam, Ithieli
na Ukali.

2 Mimi ni mjinga kuliko mtu
yeyote yule,ⁱ

Nami sina uelewaji ambao
mwanadamu anapaswa
kuwa nao.

3 Sijajifunza hekima,
Nami sina ujuzi kumhusu
Aliye Mtakatifu Zaidi.

4 Ni nani amepanda mbi-
nguni kisha akashuka?^j

Ni nani ameukusanya upe-
po katika viganja vyake
viwili?

Ni nani ameyafunga maji
katika vazi lake?^k

29:24 *Au "kiapo kinachohusisha laa-
na." **29:25** *Au "Kutetemeshwa na."
29:26 *Au labda, "kutafuta kibali cha."
Tnn., "kuutafuta uso wa."

SURA YA 29

a Est 6:6, 10
Yak 4:6

b Met 18:12
Mt 18:4
Flp 2:8, 9

c Law 5:1

d Mt 10:28
Mt 26:75

e 2Nya 14:11
Met 18:10

f Zb 62:12
Lu 18:6, 7

g Zb 119:115
Zb 139:21

h Yoh 7:7
1Yo 3:13

SURA YA 30

i Ayu 42:3

j Yoh 3:13

k Isa 40:12

Safu ya 2

a Ayu 38:4

b Zb 12:6

c Mwa 15:1
2Sa 22:31
Zb 84:11

d Kum 4:2
Ufu 22:18

e Met 12:22

f Mt 6:11
1Ti 6:8

g Kum 6:10-12

h Da 6:24

i Law 20:9
Met 19:26
Mk 7:10, 11

j Zb 36:1, 2
Isa 65:5
1Yo 1:8

Ni nani ameimarisha* mii-
sho yote ya dunia?^a

Jina lake ni nani nalo jina
la mwana wake ni nani
—ikiwa unajua?

5 Kila neno la Mungu ni
safi.^b

Yeye ni ngao kwa wale wa-
naomkimbilia.^c

6 Usiongeze chochote kati-
ka maneno yake,^d

La sivyo atakukaripia,
Nawe utathibitika kuwa
mwongo.

7 Ninakuomba mambo
mawili.

Usininyime mambo hayo
kabla sijafa.

8 Yaondolee mbali nami
mambo yasiyo ya kweli
na ya uwongo.^e

Usinipe umaskini wala
utajiri.

Acha nile tu fungu langu
la chakula,^f

9 Ili nishisibe na kukukana
na kusema, "Yehova ni
nani?"^g

Wala usiruhusu niwe
maskini, niibe na kuliai-
bisha* jina la Mungu
wangu.

10 Usimchongee mtumishi
kwa bwana wake,

La sivyo atakulaani, nawe
utapatikana na hatia.^h

11 Kuna kizazi kinachomtu-
kana baba yao

Nacho hakimbariki mama
yao.ⁱ

12 Kuna kizazi kinachojiona
kuwa safi^j

Lakini hakijasafishwa
uchafu wake.*

30:4 *Tnn., "ameinua." **30:9** *Au "ku-
lishambulia." **30:12** *Tnn., "kinyesi
chake."

13 Kuna kizazi chenye macho yaliyojaa kiburi

Na ambacho macho yake yanatazama kwa majivu-no mengi!^a

14 Kuna kizazi ambacho meno yake ni mapanga Na ambacho mataya yake ni visu vya kuchinjia; Wanawanyafua watu wa hali ya chini duniani

Na maskini kutoka miongoni mwa wanadamu.^b

15 Ruba wana mabinti wawili wanaolia, "Nipe! Nipe!"

Kuna vitu vitatu visivyotosheka,

Vinne ambavyo havisemi kamwe, "Inatosha!"

16 —Kaburi*^c na tumbo lisiloweza kuzaa,

Nchi iliyonyimwa maji, Na moto ambao kamwe hausemi, "Inatosha!"

17 Jicho linalomdhihaki baba na kudharau kumtii mama^d

—Kunguru wa bondeni* wataling'oa,

Na tai wachanga watalila.^e

18 Kuna mambo matatu yanayozidi ufahamu wangu,* Na manne ambayo siyaelewi:

19 Njia ya tai angani, Njia ya nyoka juu ya mwamba, Njia ya meli baharini, Na njia ya mwanamume pamoja na mwanamwali.

20 Hii ndiyo njia ya mwanamke mzinzi: Anakula, anajipangusa kinywa;

30:16 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. **30:17** *Au "korongoni." **30:18** *Au "ambayo ni ya ajabu sana kwangu."

SURA YA 30

a Zb 101:5
Met 6:16, 17

b Zb 14:4
Met 22:16
Isa 32:7

c Met 27:20

d Met 23:22

e Law 20:9
Kum 21:18, 21
Met 20:20

Safu ya 2

a Met 7:10, 11

b Met 19:10
Mhu 10:7
Isa 3:4

c Mwa 16:5

d Ayu 35:11

e Met 6:6-8

f Law 11:5

g Zb 104:18

h Kut 10:14
Yoe 1:4

i Yoe 2:7

j Law 11:29, 30

Kisha anasema, "Sijafanya kosa lolote."^a

21 Kuna mambo matatu yanayoitetemesha dunia Na mambo manne ambayo haiwezi kuvumilia:

22 Mtumwa anapotawala akiwa mfalme,^b

Mjinga anaposhiba kupita kiasi,

23 Mwanamke anayechukiwa* anapoolewa, Na kijakazi anapochukua nafasi ya bimkubwa wake.^c

24 Kuna vitu vinne duniani ambavyo ni miongoni mwa vitu vidogo zaidi, Lakini vina hekima ya kisi-liko:*^d

25 Chungu si viumbe wenye nguvu,* Lakini wanatayarisha chakula chao wakati wa kiangazi.^e

26 Wibari*^f si viumbe wenye nguvu,* Lakini wanajenga nyumba zao kwenye majabali.^g

27 Nzige^h hawana mfalme, Lakini wote husonga mbele kwa mpangilio.*ⁱ

28 Mjusi^j hushika kwa miguu yake, Naye huingia katika jumba la mfalme.

29 Kuna viumbe watatu wenye mwendo unaovutia, Wanne wenye mwendo wa madaha:

30 Simba, mnyama mwenye nguvu zaidi kuliko wanyama wote,

30:23 *Au "ambaye hapendwi." **30:24** *Au "hekima kupindukia." **30:25, 26** *Tnn., "si taifa lenye nguvu." **30:26** *Au "Pelele." **30:27** *Au "vikundi-vikundi."

Ambaye hamkimbii
yeyote;^a

- 31** Mbwa mwindaji; mbuzi dume;
Na mfalme aliye pamoja na jeshi lake.
- 32** Ikiwa umejikweza kwa ujinga^b
Au ikiwa umepanga kufanya hivyo,
Funika kinywa chako kwa mkono wako.^c
- 33** Kwa maana kama vile kusukasuka maziwa kunavyotokeza siagi
Na kufinya pua kunavyofanya damu itoke,
Ndivyo kuchochea hasira kunavyotokeza ugomvi.^d
- 31** Maneno ya Mfalme Lemueli, ujumbe mzito ambao mama yake alimpa ili kumfundisha:^e
- 2** Nikwambie nini, ewe mwangu,
Niseme nini, ewe mwana wa tumbo langu,
Nikwambie nini, ewe mwana wa nadhiri zangu?^f
- 3** Usiwape wanawake nguvu zako,^g
Wala kufuata njia zinazowaangamiza wafalme.^h
- 4** Si vema kwa wafalme, ewe Lemueli,
Si vema kwa wafalme kunywa divai
Wala watawala kuuliza,
“Kiko wapi kinywaji changu?”ⁱ
- 5** Ili wasinywe na kusahau maagizo
Na kupotosha haki za watu wa hali ya chini.
- 6** Wape kileo watu wanaoangamia!^j

SURA YA 30

a Hes 23:24
Isa 31:4

b Met 26:12

c Met 27:2

d Met 26:21

SURA YA 31

e Met 1:8
2Ti 1:5

f 1Sa 11:11, 28

g Ho 4:11

h Kum 17:15, 17
1Fa 11:1-3
Ne 13:26

i Mhu 10:17
Isa 28:7

j Zb 104:15
Mt 27:34

Safu ya 2

a Yer 16:7

b Zb 82:4

c Kum 1:16, 17
2Sa 8:15
Zb 72:1, 2
Isa 11:4

d Ru 3:10, 11
Met 12:4
Met 19:14

e 1Sa 2:18, 19
Tit 2:3-5

f 2Nya 9:21

Na divai wale wanaoteseka vikali.^{*a}

- 7** Acha wanywe na kusahau umaskini wao;
Na wasikumbuke tena taabu yao.
- 8** Watete wasioweza kuzungumza;
Tetea haki za wote wanaoangamia.^b
- 9** Sema waziwazi na uhukumu kwa uadilifu;
Tetea haki za^{*} watu wa hali ya chini na maskini.^c
‡ [Aleph]
- 10** Ni nani anayeweza kumpata mke mwema?^{*d}
Thamani yake inazidi kabisa thamani ya marijani.[#]
‡ [Beth]
- 11** Mume wake humwamini kutoka moyoni,
Na mume huyo hakosi chochote chenye thamani.
‡ [Gimel]
- 12** Humthawabisha mume wake kwa mema, wala si kwa mabaya,
Sikuzote za maisha yake.
‡ [Daleth]
- 13** Hujipatia safu na kitani;
Hufurahia kufanya kazi kwa mikono yake.^e
‡ [He]
- 14** Yeye ni kama meli za mfanabiashara,^f
Huleta chakula chake kutoka mbali.
‡ [Waw]
- 15** Pia yeye huamka kabla ya mapambazuko,
Na kuwaandalia chakula watu wa nyumbani mwake
- 31:6** *Au “wenye uchungu nafsi.”
31:9 *Au “Tetea kesi ya.” **31:10** *Au “mwenye uwezo; bora.” #Angalia Kamusi, uku. 2012.

- Na kuwapa mafungu vija-kazi wake.^a
 † [Zayin]
- 16 Hulikazia fikira shamba na kulinunua;
 Hupanda shamba la miza-bibu kwa jasho lake.*
 † [Heth]
- 17 Hujitayarisha kwa ajili ya kazi ngumu,^{*b}
 Naye huitia nguvu mikono yake.
 † [Teth]
- 18 Huhakikisha kwamba biashara yake ina faida;
 Taa yake haizimiki usiku.
 * [Yod]
- 19 Mikono yake hushika kijiti cha kusokotea uzi,
 Na mikono yake hushika gurudumu la mfumaji.^c
 † [Kaph]
- 20 Humnyooshea mkono mtu wa hali ya chini,
 Huwafumbulia maskini mikono yake.^d
 † [Lamed]
- 21 Wakati wa theluji hana wasiwasi kuhusu watu wa nyumbani mwake,
 Kwa sababu watu wote wa nyumbani mwake wamevaa mavazi yenye joto.*
 † [Mem]
- 22 Hujitengenezea matandiko ya kufunika kitanda.
 Mavazi yake ni ya kitani za safu ya zambarau.
 † [Nun]
- 23 Mume wake anajulikana sana kwenye malango ya jiji,^e
 Ambapo huketi pamoja na wazee wa nchi.

31:16 *Au "kwa mapato yake." Tnn., "kutokana na matunda ya mikono yake."
 31:17 *Tnn., "Hufunga nguvu kiunoni mwake."
 31:21 *Tnn., "mavazi mawili-mawili."

SURA YA 31

a 1Ti 5:9, 10

b Mwa 24:15, 20

c Kut 35:25

d 1Sa 25:18
Met 19:17
1Ti 2:10
Ebr 13:16e Ru 4:1
Ayu 29:7, 8

Safu ya 2

a Amu 13:22, 23
1Sa 25:30, 31
Est 5:8
Tit 2:3b Met 14:1
1Ti 5:9, 10
Tit 2:3-5c 2Fa 9:30
Est 1:10-12
Met 6:25, 26d Mwa 24:60
Amu 5:7
1Pe 3:3, 4

e Ru 3:10, 11

f Ro 16:1, 2

‡ [Samekh]

- 24 Hufuma nguo za kitani* na kuziua
 Na kuwauzia mishipi wafanyabiashara.
 † [Ayin]
- 25 Amevaa nguvu na fahari, Naye huutamia wakati ujao kwa uhakika.*
 † [Pe]
- 26 Hufumbua kinywa chake kwa hekima;^a
 Sheria ya fadhili iko* kwenye ulimi wake.
 † [Tsade]
- 27 Huangalia shughuli za nyumbani mwake,
 Naye hali mkate wa uvivu.^b
 † [Qoph]
- 28 Watoto wake husimama na kumtanza kuwa mwenye furaha;
 Mume wake husimama na kumsifu.
 † [Resh]
- 29 Kuna wanawake wengi walio wema,*
 Lakini wewe—wewe ume-wapita wote hao.
 † [Shin]
- 30 Sura nzuri inaweza kudanganya, na huenda urembo ukatoweka upesi,^{*c}
 Lakini mwanamke anayemwogopa Yehova atasifiwa.^d
 † [Taw]
- 31 Mpeni thawabu kwa mambo anayofanya,^{*e}
 Kazi zake na zimsifu kwenye malango ya jiji.^f

31:24 *Au "nguo za ndani." 31:25 *Au "huucheka wakati ujao." 31:26 *Au "Mafundisho ya upendo yako; Sheria ya upendo mshikamanifu iko." 31:29 *Au "mwenye uwezo; bora." 31:30 *Au "ukawa ubatili." 31:31 *Tnn., "Mpeni baadhi ya matunda ya mikono yake."

MHUBIRI

YALIYOMO

- 1 Kila kitu ni ubatili (1-11)
 - Dunia inadumu milele (4)
 - Mizunguko ya asili huendelea (5-7)
 - Hakuna jambo jipya chini ya jua (9)Hekima ya wanadamu ni duni (12-18)
 - Kukimbiza upepo (14)
- 2 Maelezo kuhusu mambo aliyotimiza Sulemani (1-11)
 - Hekima ya wanadamu haina faida kubwa (12-16)
 - Ubatili wa kazi ya jasho (17-23)
 - Ule, unywe, na kufurahia kazi (24-26)
- 3 Kila jambo lina wakati wake (1-8)
 - Kufurahia maisha ni zawadi kutoka kwa Mungu (9-15)
 - Umilele umo ndani ya mioyo ya wanadamu (11)
 - Mungu huwahukumu wote kwa haki (16, 17)
 - Wanadamu na wanyama wote hufa (18-22)
 - Wote watarudi mavumbini (20)
- 4 Ukandamizaji ni mbaya kuliko kifo (1-3)
 - Maoni yanayofaa kuhusu kazi (4-6)
 - Faida ya rafiki (7-12)
 - Wawili ni bora (9)
 - Maisha ya mtawala yanaweza kuwa ya ubatili (13-16)
- 5 Mkaribie Mungu kwa woga unaofaa (1-7)
 - Walio chini hutazamwa na walio juu zaidi (8, 9)
 - Ubatili wa utajiri (10-20)
 - Wanaopenda pesa hawatosheki kamwe (10)
 - Usingizi wa mfanyakazi ni mtamu (12)
- 6 Mali bila furaha (1-6)
 - Furahia ulicho nacho (7-12)
- 7 Jina zuri na siku ya kufa (1-4)
 - Kemeo la mtu mwenye hekima (5-7)
 - Mwisho ni bora kuliko mwanzo (8-10)
 - Faida ya hekima (11, 12)
- Siku njema na siku mbaya (13-15)
 - Usipite kiasi (16-22)
 - Aliyoyaona mkutanishaji (23-29)
- 8 Mwanadamu asiye mkamilifu anapotawala (1-17)
 - Tii amri za mfalme (2-4)
 - Madhara ya utawala wa mwanadamu (9)
 - Hukumu isipotekelezwa upesi (11)
 - Ule, unywe, na kufurahia (15)
- 9 Wote hupatwa na jambo lilelile (1-3)
 - Furahia maisha licha ya kwamba utakufa (4-12)
 - Waliokufa hawajui jambo lolote (5)
 - Hakuna kazi yoyote Kaburini (10)
 - Wakati na matukio yasiyotarajiwa (11)
 - Hekima haithaminiwi sikuzote (13-18)
- 10 Upumbavu kidogo huharibu hekima (1)
 - Hatari za upumbavu (2-11)
 - Madhara ya kuwa mjinga (12-15)
 - Upumbavu miongoni mwa watawala (16-20)
 - Huenda ndege akarudia maneno uliyosema (20)
- 11 Tumia fursa unayopata (1-8)
 - Tupa mkate wako juu ya maji (1)
 - Panda mbegu kuanzia asubuhi mpaka jioni (6)
 - Furahia ujana wako kwa njia inayofaa (9, 10)
- 12 Mkumbuke Muumba kabla hujazeeka (1-8)
 - Hitimisho la maneno ya mkutanishaji (9-14)
 - Maneno ya hekima ni kama michokoo ya kuongozea ng'ombe (11)
 - Mwogope Mungu wa kweli (13)

1 Maneno ya mkutanishaji,^a mwana wa Daudi, mfalme wa Yerusalemu.^b

2 “Ubatili mkubwa kupita wote!” asema mkutanishaji,

“Ubatili mkubwa kupita wote! Kila kitu ni ubatili!”^c

3 Mtu hupata faida gani kutokana na kazi yake yote ngumu

Anayofanya kwa jasho chini ya jua?^d

4 Kizazi huenda, na kizazi huja, Lakini dunia inadumu* milele.^e

5 Jua huchomoza, * na jua hutua; Kisha hurudi haraka^f mahali linapochomozea tena.^f

6 Upepo huelekea kusini na kuzungukazunguka hadi kaskazini;

Huendelea kuzungukazunguka; upepo huendelea na mizunguko yake.

7 Vijito vyote* hutiririka kuingia baharini, lakini bado bahari haijai.^g

Mahali vijito vinakotoka, huko ndiko vinakorudi ili vitiririke tena.^h

8 Mambo yote yanachosha sana;

Hakuna yeyote anayeweza hata kueleza jambo hilo.

Jicho halitosheki kuona; Wala sikio halishibi ku-sikia.

1:1 *Au “yule anayewakusanya watu; mhubiri.” 1:4 *Tnn., “inasimama.” 1:5 *Au “huangaza.” #Au “hurudi likihemahema.” 1:7 *Au “Vijito vyote vya majira ya baridi kali; Vijito vyote vya majira.”

SURA YA 1

a 1Fa 8:1, 22

b 1Fa 2:12
2Nya 9:30

c Zb 39:5
Ro 8:20

d Mhu 2:11
Mt 16:26
Yoh 6:27

e Zb 78:69
Zb 104:5
Zb 119:90

f Mwa 8:22
Zb 19:6

g Ayu 38:8, 10

h Ayu 36:27, 28
Isa 55:10
Amo 5:8

Safu ya 2

a Mwa 8:22
Mhu 1:4

b Mhu 2:16
Mhu 9:5
Isa 40:6

c 1Fa 11:42
Mhu 1:1

d 1Fa 4:29, 30

e Mhu 8:16

f Zb 39:5, 6
Mhu 2:11, 18
Mhu 2:26
Lu 12:15

g Mhu 2:9

h 1Fa 3:28
1Fa 4:29-31
2Nya 1:10-12

9 Jambo ambalo limekuwako, ndilo litakalokuwako, Na jambo ambalo limefanywa, litafanywa tena; Hakuna jambo jipya chini ya jua.^a

10 Je, kuna jambo lolote ambalo mtu anaweza kusema, “Tazama jambo hili—ni jipya?”

Tayari lilikuwako tangu zamani za kale;

Lilikuwako kabla ya wakati wetu.

11 Hakuna yeyote anayewakumbuka watu wa zamani;

Wala hakuna yeyote atakayewakumbuka watako-kuja baadaye;

Wala hawatakumbukwa na wale watako-kuja hata baadaye.^b

12 Mimi, mkutanishaji, nimekuwa mfalme wa Israeli huko Yerusalemu.^c **13** Nilia-zimia moyoni mwangu kujifunza na kuchunguza kwa hekima^d kila jambo ambalo limefanywa chini ya mbingu^e—kazi ya kusikitisha ambayo Mungu amewapa wanadamu inayofanya waendeleo kushughulika.

14 Niliona kazi zote zilizofanywa chini ya jua, Na, tazama! kila jambo lilikuwa ubatili, kukimbiza upepo.^f

15 Kilichopinda hakiwezi kunooshwa, Na kisichokuwapo huenda kisiweze kuhesabiwa.

16 Kisha nikasema moyoni mwangu: “Tazama! Nimepata hekima nyingi, kuliko mtu yeyote aliyenitangulia Yerusalemu,^g na moyo wangu ulipata hekima nyingi sana na ujuzi.”^h

17 Nilijitahidi sana ili moyo wangu ujue hekima na kujua wazimu* na kujua ujinga,^a na hilo pia ni kukimbiza upepo.

18 Kwa maana hekima nyingi humfanya mtu azidi kukata tamaa,

Hivi kwamba yeyote anayeongeza ujuzi anaongeza maumivu.^b

2 Kisha nikasema moyoni mwangu: "Haya, acha nija-ribu starehe,* nione ni jambo gani jema litakalokuja." Lakini tazama! hilo pia lilikuwa ubatili.

2 Nilisema hivi kuhusu kicheko: "Ni wazimu!"

Na kuhusu starehe,* "Ina faida gani?"

3 Nilijaribu kuufurahisha moyo wangu kwa divai,^c huku nikielelea kuwa na hekima yangu; hata nilikumbatia ujinga ili nione jambo bora ambalo wanadamu wanapaswa kufanya katika siku chache wanaoishi chini ya mbingu.

4 Nilianza kufanya mambo makubwa.^d Nikajijengea nyumba;^e Nikajipandia mashamba ya mizabibu.^f **5** Nikajitengezeza mashamba na bustani, na humo nikapanda miti ya matunda ya kila aina. **6** Nikajichimbua mabwawa ya maji, ili kumwagilia maji msitu wenyewe miti iliyokuwa ikisitawi.

7 Nikapata watumishi wa kiume na wa kike,^g na watumishi wengine walizaliwa nyumbani mwangu.* Pia, nilipata mifugo mingi—ng'ombe na kondoo na mbuzi^h—kuliko mtu yeyote aliyenitangulia Yerusale-

1:17 *Au "upumbavu wa kupindukia." 2:1 *Au "kushangilia." 2:2 *Yaani, kushangilia. 2:7 *Tnn., "na nilikuwa na wana wa nyumba."

SURA YA 1

a Mhu 2:2, 3
Mhu 2:12
Mhu 7:25

b Mhu 2:15
Mhu 12:12

SURA YA 2

c Zb 104:15
Mhu 10:19

d 1Fa 9:17-19
2Nya 9:15, 16

e 1Fa 7:1, 8

f 1Fa 4:25
Wim 8:11

g 1Sa 8:10, 13
1Fa 9:22

h 1Fa 4:22, 23

Safu ya 2

a 1Fa 9:14, 28
1Fa 10:10
2Nya 1:15

b 1Fa 10:14, 15
2Nya 9:13, 14

c 1Fa 3:13
1Fa 10:23

d Mhu 11:9

e Mhu 3:22
Mhu 5:18
Mhu 9:9

f 1Fa 7:1

g Zb 49:10
Mhu 1:14
Mhu 2:16
1Ti 6:7

h Mhu 1:3
Mhu 2:17

i Mhu 1:17
Mhu 7:25

j Met 4:7
Mhu 7:11, 12

k Met 4:25

l Met 14:8
Met 17:24
Yoh 3:19
1Yo 2:11

mu. **8** Nikajikusanyia fedha na dhahabu,^a hazina za* wafalme na za mikoa.^b Nikajikusanyia waimbaji wa kiume na wa kike, na pia chanzo cha raha tele kwa wanaume—mwanaume, naam, wanawake wengi. **9** Basi nikawa mkuu, nikamzidi mtu yeyote aliyenitangulia Yerusalemu.^c Nami nikaendelea kuwa na hekima yangu.

10 Sikujinyima chochote nilichotamani.*^d Sikuuunyima moyo wangu raha^e yoyote ile, kwa maana moyo wangu ulishangilia kwa sababu ya kazi yangu yote ngumu, na hiyo ndiyo iliyokuwa thawabu yangu^f kwa sababu ya kazi yangu yote ngumu.^e **11** Lakini nilipofikiria kazi zote nilizofanya kwa mikono yangu mwenyewe na kazi yangu yote ngumu niliyofanya kwa jasho ili kuitimiza,^f niliona kwamba kila kitu kilikuwa ubatili, kukimbiza upepo;^g hakukuwa na kitu chochote chenye thamani ya kweli* chini ya jua.^h

12 Basi nikaanza kuchunguza hekima na wazimu na ujinga.ⁱ (Kwa maana mtu anayekuja baada ya mfalme anaweza kufanya nini? Anaweza kufanya tu jambo ambalo tayari limefanywa.) **13** Nami nikao-na kwamba hekima ina faida kuliko ujinga,^j kama tu nuru ilivyo na faida kuliko giza.

14 Mtu mwenye hekima ana macho kichwani mwake;^k lakini mpumbavu anatembea gizani.^l Pia nimegundua kwamba wote wana mwisho uleu-

2:8 *Au "mali ambazo kwa kawaida ni za." 2:10 *Tnn., "ambacho macho yangu yaliomba." #Au "shangwe." ^Au "na hilo ndilo lililokuwa fungu langu." 2:11 *Au "manufaa." 2:14 *Au "anafungua macho yake."

le.*^a **15** Kisha nikasema moyoni mwangu: "Kinachompa ta mpumbavu ndicho kitakachonipata mimi pia."^b Sasa, basi, nilipata faida gani kwa kuwa na hekima kupita kiasi? Basi nikasema moyoni mwangu: "Hili pia ni ubatili."

16 Kwa maana hakuna atakayekumbukwa daima, iwe ni mwenye hekima au mpumbavu.^c Siku zijazo, kila mtu atasahauliwa. Na mwenye hekima atakufa jinsi gani? Pamoja na mpumbavu.^d

17 Basi nikachukia maisha,^e kwa sababu kila jambo linalofanywa chini ya jua lilionekana kwangu kuwa lenye kuhuzunisha, kwa sababu kila jambo lilikuwa ubatili,^f kukimbiza upepo.^g **18** Nikachukia vitu vyote nilivyokuwa nimefanya kazi ngumu chini ya jua ili kupipata,^h kwa sababu ni lazima nimwachie mtu atakaye-kuja baada yangu.ⁱ **19** Na ni nani anayejua ikiwa atakuwa mwenye hekima au mjinga? Lakini bado atamiliki vitu vyote nilivyotafuta kwa jitihada nyingi na hekima chini ya jua. Hilo pia ni ubatili. **20** Basi nikaanza kukata tamaa moyoni mwangu kwa sababu ya kazi yangu yote ngumu niliyofanya kwa jasho chini ya jua. **21** Kwa maana mtu anaweza kufanya kazi kwa bidii, akiongozwa na hekima na ujuzi na ustadi, lakini ni lazima amwachie fungu lake mtu ambaye hakulifanyia kazi.*^k Hili pia ni ubatili na ni msiba mkubwa.*

22 Kwa kweli mtu hupata faida gani kutokana na kazi yake yote ngumu na ta-

2:14 *Au "hatima ileile." 2:21 *Au "ampe vitu vyote mtu ambaye hakulifanyia kazi." *Au "janga kubwa."

SURA YA 2

a Mhu 3:19, 20

Mhu 9:2, 3
Mhu 9:11

b Zb 49:10

c Kut 1:8

Mhu 1:11

d Mhu 6:8

Ro 5:12

e 1Fa 19:2, 4

Yer 20:17, 18

f Ayu 7:6

Mhu 2:21

Ro 8:20

g Mhu 1:14

Mhu 5:16

h Mhu 2:4-8

i Zb 39:6

Lu 12:20

j 1Fa 12:6, 8

2Nya 12:1, 9

k Mhu 2:18

Mhu 5:15, 16

Safu ya 2

a Mhu 1:3

Mhu 3:9

b Ayu 14:1, 2

Lu 12:29

c Mwa 31:40, 41

d Kum 12:18

Mhu 3:22

Mhu 8:15

Mdo 14:17

e Mhu 3:12, 13

Mhu 5:18, 19

f 1Fa 4:7

1Fa 4:22, 23

1Fa 10:4, 5

1Fa 10:21

g 1Sa 18:14

Met 3:32, 33

Isa 3:10

h Kum 6:10, 11

Met 13:22

Met 28:8

maa inayomchochea* kufanya kazi kwa bidii chini ya jua?^a

23 Kwa maana siku zake zote, kazi yake humletea maumivu na kumkatisha tamaa,^b na hata usiku moyo wake haupumziki.^c Hili pia ni ubatili.

24 Hakuna jambo bora analoweza kufanya mtu kuliko kula na kunywa na kufurahia* kazi yake ngumu.^d Hili pia nimegundua kwamba linatoka mkononi mwa Mungu wa kweli,^e **25** kwa maana ni nani anayekula na ni nani anayekunywa vizuri kuliko mimi?^f

26 Yeye humpa mtu anayempendeza hekima na ujuzi na shangwe,^g lakini humpa mte nda dhambi kazi ya kukusanya na kurundika tu, ili ampe yule anayempendeza Mungu wa kweli.^h Hili pia ni ubatili, kukimbiza upepo.

3 Kuna wakati uliowekwa wa kila jambo,

Wakati wa kila shughuli chini ya mbingu:

2 Wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa;

Wakati wa kupanda na wakati wa kung'oa kilichopandwa;

3 Wakati wa kuua na wakati wa kuponya;

Wakati wa kubomoa na wakati wa kujenga;

4 Wakati wa kulia na wakati wa kucheka;

Wakati wa kuomboleza kwa sauti na wakati wa kucheza dansi;*

5 Wakati wa kutupa mawe na wakati wa kukusanya mawe;

2:22 *Tnn., "jitihada za moyo wake za."

2:24 *Au "kuifanya nafsi yake ione mema kwa sababu ya." 3:4 *Tnn., "kuruka; kururuka."

Wakati wa kukumbatia na wakati wa kuacha kukumbatia;

6 Wakati wa kutafuta na wakati wa kuacha kutafuta kilichopotea;

Wakati wa kuhifadhi na wakati wa kutupa;

7 Wakati wa kurarua^a na wakati wa kushona,

Wakati wa kunyamaza^b na wakati wa kuongea;^c

8 Wakati wa kupenda na wakati wa kuchukia;^d

Wakati wa vita na wakati wa amani.

9 Mfanyakazi hupata faida gani kutokana na jitihada zake zote?^e **10** Nimeona kazi ambayo Mungu amewapa wanadamu wajishughulishaye nayo. **11** Amefanya kila kitu kipendeze* kwa wakati wake.^f Hata ameweka umilele katika moyo wao; lakini bado wanadamu hawatajua kamwe kazi ambayo Mungu wa kweli amefanya tangu mwanzo mpaka mwisho.

12 Nimefikia mkataa kwamba hakuna jambo bora wanaloweza kufanya kuliko kushangilia na kufanya mema maishani mwao,^g **13** na kwamba kila mtu anapaswa kula na kunywa na kufurahia kazi yake yote ngumu. Ni zawadi kutoka kwa Mungu.^h

14 Sasa nimejua kwamba kazi zote za Mungu wa kweli zitadumu milele. Hakuna chochote kinachoweza kuongezwa wala chochote kinachoweza kupunguzwa kwenye kazi zake. Mungu wa kweli amezifanya ziwe hivyo, ili watu wamwogope.ⁱ

3:11 *Au "kiwe na mpangilio mzuri; kifae."

SURA YA 3

a 2Sa 3:31

b Zb 39:1

c 1Sa 19:4
1Sa 25:23, 24
Est 4:13, 14
Zb 145:11
Met 9:8

d Zb 139:21
Ro 12:9

e Mhu 1:3
Mhu 5:15, 16

f Mwa 1:31
Ro 1:20

g Zb 37:3
1Th 5:15

h Mhu 5:18, 19
Isa 65:21, 22

i Yer 10:7
Ufu 15:4

Safu ya 2

a Mhu 1:9

b Zb 82:2
Zb 94:16, 21

c Mhu 12:14
Mdo 17:31
Ro 2:5, 6

d Ayu 14:10
Zb 39:5
Zb 89:48

e Mwa 7:22
Zb 104:29
Mhu 12:7

f Mhu 9:10

g Mwa 2:7, 19

h Mwa 3:19
Ayu 10:9

i Zb 146:3, 4
Mhu 3:19
Mhu 9:10

j Kum 12:7
Mhu 5:18

k Ayu 14:21
Mhu 6:12

15 Jambo lolote linalotukia limewahi kutukia, na litakalokuja limewahi kuwepo;^a lakini Mungu wa kweli hutafuta kilichofuatiwa.*

16 Pia nimeona jambo hili chini ya jua: Badala ya haki kulikuwa na uovu, na badala ya uadilifu kulikuwa na uovu.^b

17 Basi nikasema moyoni mwangu: "Mungu wa kweli atawahukumu waadilifu na waovu,^c kwa maana kuna wakati kwa ajili ya kila kazi na kila tendo."

18 Pia nikasema moyoni mwangu kwamba Mungu wa kweli atawajaribu wanadamu na kuwaonyesha kwamba wao ni kama wanyama, **19** kwa maana kuna mwisho wa* wanadamu na mwisho wa wanyama; wote wana mwisho uleule.^d Anavyokufa huyu, ndivyo anavyokufa huyu; na wote wana roho ileile.^e Kwa hiyo mwanadamu si bora kuliko wanyama, kwa maana kila kitu ni ubatili. **20** Wote wanaenda mahali palepale.^f Wote wanatoka mavumbini,^g na wote wanarudi mavumbini.^h

21 Kwa kweli ni nani anayejua ikiwa roho ya wanadamu hupanda kwenda juu, na ikiwa roho ya wanyama hushuka chini ardhini?ⁱ **22** Nami nikaona kwamba hakuna jambo bora kwa mwanadamu kuliko kufurahia kazi yake,^j kwa sababu hiyo ndiyo zawadi yake;* kwa maana ni nani anayeweza kumwezesha aone yatakayotukia baada ya kifo chake?^k

4 Tena, nikakazia uangalifu matendo yote ya ukandamizaji yanayofanywa chi-

3:15 *Au labda, "kilichopitilia mbali."
3:19 *Au "hatima ya." 3:22 *Au "hilo ndilo fungu lake."

ni ya jua. Nikaona machozi ya wanaokandamizwa, na haku-kuwa na mtu yeyote wa ku-wafariji.^a Na wale waliowakan-damiza walikuwa na nguvu, lakini waliokandamizwa ha-wakuwa na mtu yeyote wa ku-wafariji. **2** Nami nikawapongeza wafu ambao tayari walikuwa wamekufa badala ya walio hai ambao bado waliku-wa hai.^b **3** Na yule ambaye hajazaliwa ni afadhali kuliko hao wawili,^c kwa kuwa hajao-na mambo yenye kuhuzunisha yanayofanywa chini ya jua.^d

4 Nami nimeona jinsi ambavyo uhindani kati ya watu unavyowafanya wajitahidi sana* na kufanya kazi kwa ustadi;^e hili pia ni ubatili, kukimbiza upepo.

5 Mpumbavu hukunja mikonu yake huku mwili wake ukiendelea kudhoofika.*^f

6 Ni afadhali konzi moja ya pumziko kuliko konzi mbili za kazi ngumu na kukimbiza upepo.^g

7 Nilikazia uangalifu mfano mwingine wa ubatili chini ya jua: **8** Kuna mtu aliye peke yake, asiye na rafiki yeyote; hana mwana wala ndugu, lakini kazi yake yote ngumu haina mwisho. Macho yake hayatosheki kamwe na utajiri.^h Lakini je, yeye hujiuliza, 'Ninafanya kazi kwa bidii na kujinyima* vitu vyema kwa ajili ya nani?'ⁱ Hili pia ni ubatili na ni kazi inayosikitisha.^j

9 Wawili ni afadhali kuliko mmoja^k kwa sababu wanapata thawabu njema* kwa kazi

4:4 *Au "wajitahidi kufanya kazi ya jasho." 4:5 *Tnn., "naye anakula mwili wake mwenyewe." 4:8 *Au "kuinyima nafsi yangu." 4:9 *Au "faida kubwa zaidi."

SURA YA 4

a Zb 69:20
Zb 142:4

b Ayu 3:17
Mhu 2:17

c Yer 20:18

d Mhu 1:14

e Gal 5:26

f Met 6:10, 11
Met 20:4

g Zb 37:16
Met 15:16
Met 16:8
Met 17:1

h Met 27:20
Mhu 5:10

i Zb 39:6
Lu 12:18-20

j Mhu 2:22, 23

k Mwa 2:18
Met 27:17

Safu ya 2

a Met 19:1
Met 28:6, 16

b 1Fa 22:8
2Nya 25:15, 16

c Mwa 41:14, 40

d 2Sa 7:8
Ayu 5:11

e 2Sa 20:1

SURA YA 5

f Zb 15:1, 2

g Kum 31:12
Mdo 17:11

h 1Sa 13:12, 13
1Sa 15:22
Met 21:27
Isa 1:13
Ho 6:6

yao ngumu. **10** Kwa maana mmoja wao akianguka, mwenzake anaweza kumwinua. Lakini itakuwaje kwa yule atakayeanguka naye hana mtu wa kumwinua?

11 Tena, wawili wakilala pamoja, watapata joto, lakini mtu mmoja tu atapata joto? **12** Na mtu anaweza kumzidi nguvu aliye peke yake, lakini wawili walio pamoja wanaweza kukabiliana naye. Na kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi.*

13 Ni afadhali mtoto maskini lakini mwenye hekima kuliko mfalme mzee lakini mpumbavu,^a ambaye hana tena ufahamu wa kutosha wa kutii onyo.^b **14** Kwa maana alitoka* gerezani ili awe mfalme,^c ingawa alizaliwa maskini katika utawala wa mfalme huyo.^d **15** Niliwafikiria wote walio hai wanaotembeatembea chini ya jua, na pia hali ya yule mta-wala kijana anayechukua mahali pa yule mfalme. **16** Inga-wa idadi ya wafuasi wake wote haina mwisho, wale watako-kuja baadaye hawatafurahishwa naye.^e Hili pia ni ubatili, kukimbiza upepo.

5 Uwe mwangalifu* wakati wowote unapoenda katika nyumba ya Mungu wa kweli;^f ni afadhali ukaribie ili kusikiliza^g badala ya kutoa dhambi-hu kama wanavyofanya wapumbavu,^h kwa maana hawajui kwamba jambo wanalofanya ni baya.

2 Usifungue kinywa chako haraka, wala usiruhusu moyo wako uzungumze bila kufikiri

4:12 *Au "kwa urahisi." 4:14 *Labda ni yule mtoto mwenye hekima. 5:1 *Au "Chunga hatua zako."

mbele za Mungu wa kweli,^a kwa maana Mungu wa kweli yuko mbinguni lakini wewe uko duniani. Ndiyo sababu maneno yako yanapaswa kuwa machache.^b **3** Kwa maana ndoto huja kwa sababu ya shughuli nyingi sana,^c na mpumbavu huropoka kwa sababu ya kuwa na maneno mengi sana.^d **4** Wakati wowote unapoweka nadhiri kwa Mungu,^e usikawie kuitimiza, kwa maana hapendezwi na wapumbavu.^f Unapoweka nadhiri, itimize.^g **5** Ni afadhali usiweke nadhiri kuliko kuweka nadhiri na kukosa kuitimiza.^h **6** Usiruhusu kinywa chako kikufanye* utende dhambi,ⁱ wala usiseme mbele ya malaika[#] kwamba nilikosea.^j Kwa nini umkasirishe Mungu wa kweli kwa yale unayosema hivi kwamba alazimike kuharibu kazi ya mikono yako?^k **7** Kwa maana kama vile shughuli nyingi zinavyomfanya mtu aote ndoto,^l vivyo hivyo, maneno mengi huongoza kwenye ubatili. Lakini mwoyope Mungu wa kweli.^m

8 Ukiona maskini wakikandamizwa kwa njia yoyote ile na haki na uadilifu zikikiukwa katika wilaya yenu, usishangazwe na jambo hilo.ⁿ Kwa maana ofisa huyo mkuu anatazama na yule aliye juu zaidi yake, na kuna wengine walio juu zaidi yao.

9 Pia, faida ya nchi hugawanywa miongoni mwao wote; hata mfalme huhudumiwa kutokana na shamba hilo.^o

10 Anayependa fedha hatatosheka na fedha, wala ana-

5:3 *Au "mahangaiko mengi sana." 5:6 *Tnn., "mwili wako ukufanye." #Au "mjumbe."

SURA YA 5

a Hes 30:2
1Sa 14:24

b Met 10:19

c Mt 6:25, 34
Lu 12:18-20

d Met 10:19
Met 15:2

e Kum 23:21
Zb 76:11
Mt 5:33

f Mhu 10:12

g Hes 30:2
Zb 66:13

h Kum 23:22
Met 20:25

i Amu 11:35

j Law 5:4

k Zb 127:1
Hag 1:11

l Mhu 5:3

m Mhu 12:13

n Mhu 3:16

o 1Sa 8:11, 12
1Fa 4:7
2Nya 26:9, 10
Wim 8:11

Safu ya 2

a Mhu 4:8

b Mt 6:24
Lu 12:15
1Ti 6:10

c 1Fa 4:22, 23

d Met 23:4, 5
1Yo 2:16

e Met 23:4, 5
Mt 6:19

f Ayu 1:21

g Zb 49:17
Lu 12:20
1Ti 6:7

h Mt 16:26
Yoh 6:27

i 1Ti 6:10

j 1Fa 4:20

k Mhu 2:24
Mhu 3:22
Isa 65:21, 22

yependa mali hatatosheka na mapato.^a Hili pia ni ubatili.^b

11 Vitu vizuri vinapoongezeka, walaji huongezeka.^c Na mwenye vitu hivyo hupata faida gani, ila kuviangalia tu kwa macho yake?^d

12 Usingizi wa mtumishi ni mtamu, iwe anakula kidogo au kingi, lakini wingi alionao taji-ri haumruhusu kulala usingizi.

13 Kuna msiba mkubwa ambao* nimeona chini ya jua: utajiri uliorundikwa na mtu na kumdhuru yeye mwenyewe. **14** Utajiri huo ulipoteka kwa sababu ya mradi ambao haukufanikiwa,* na anapomzaa mwana, habaki na kitu chochote.^e

15 Kama mtu alivyotoka katika tumbo la mama yake akiwa uchi, ndivyo atakavyoenda, kama alivyokuja.^f Naye hawezi kwenda na chochote alichopata kutokana na kazi yake yote ngumu.^g

16 Huu pia ni msiba mkubwa:* Kama tu alivyokuja, ndivyo atakavyoenda; na mtu ambaye anafanya kazi kwa bidii daima kwa ajili ya upepo anapata faida gani?^h **17** Pia, yeye hula gizani kila siku, akiwa amekata tamaa kabisa na akiwa mgonjwa na akiwa amekasirika kabisa.ⁱ

18 Hili ndilo jambo ambalo nimeona ni jema na linafaa: kwamba mtu anapaswa kula na kunywa na kufurahia kazi yote ngumu/ anayofanya kwa jasho chini ya jua katika siku chache za maisha alizopewa na Mungu wa kweli, kwa maana hiyo ndiyo thawabu yake.*^k

5:13 *Au "janga kubwa ambalo." 5:14 *Tnn., "kazi ya msiba." 5:16 *Au "Hili pia ni janga kubwa." 5:18 *Au "hilo ndilo fungu lake."

19 Pia, Mungu wa kweli anapompa mtu utajiri na mali^a pamoja na uwezo wa kufurahia vitu hivyo, anapaswa kuchukua thawabu yake* na kushangilia katika kazi yake ngumu. Hiyoni ndiyo zawadi kutoka kwa Mungu.^b **20** Kwa maana hataona* kwa urahisi jinsi siku za maisha yake zinavyopita, kwa sababu Mungu wa kweli humshughulisha na shangwe ya moyo wake.^c

6 Kuna msiba mwingine* ambao nimeona chini ya jua, nao ni wa kawaida miongoni mwa wanadamu: **2** Mungu wa kweli humpa mtu utajiri na mali na utukufu, hivi kwamba hakosi chochote anachotamani;* lakini Mungu wa kweli hamwezeshi kuvifurahia, ingawa mgeni anaweza kuvifurahia. Hili ni ubatili na ni mateso makali. **3** Mtu akizaa watoto mia moja, aishi miaka mingi na kuzee-ka, lakini hafurahii vitu vyake vizuri kabla hajaingia kaburini, sina budi kusema kwamba mtoto aliyefia tumboni ni afadhali kuliko mtu huyo.^d **4** Kwa maana mtoto huyo alikuja bure na kwenda zake gizani, na jina lake limetokomea gizani. **5** Hata ingawa hakuwahi kuliona jua wala kujua kitu chochote, yeye bado ni afadhali* kuliko mtu huyo.^e **6** Kuna faida gani ya kuishi miaka elfu moja mara mbili lakini bila furaha? Je, wote hawaendi mahali pale-pale?^f

5:19 *Au "fungu lake." 5:20 *Au "hatakumbuka." 6:1 *Au "janga lingine." 6:2 *Au "hakosi chochote kwa ajili ya nafsi yake." 6:5 *Tnn., "ana pumziko zaidi."

SURA YA 5

a 1Fa 3:12, 13
Ayu 42:12

b Kum 8:10
Mhu 3:12, 13
1Ti 6:17
Yak 1:17

c Kum 28:8
Zb 4:7

SURA YA 6

d Mhu 4:2, 3

e Ayu 3:11, 13
Ayu 14:1

f Ayu 30:23
Mhu 3:20
Ro 5:12

Safu ya 2

a Mwa 3:19
Met 16:26

b Zb 49:10
Mhu 2:15, 16

c 1Nya 29:15
Ayu 8:9
Ayu 14:1, 2
Zb 102:11

SURA YA 7

d Met 10:7
Met 22:1
Isa 56:5
Lu 10:20

e Isa 5:11, 12

7 Kazi yote ngumu ambayo mtu hufanya ni kwa ajili ya kujaza kinywa chake;^a na bado hamu* yake haitoshelezwi kamwe. **8** Kwa maana mwenye hekima anamzidi mpumbavu kwa njia gani,^b au maskini hupata faida gani akijua jinsi ya kukabiliana na maisha?^{*c} **9** Ni afadhali mtu afurahie mambo ambayo macho yanaona kuliko kutangatanga akifuatia tamaa zake.* Hili pia ni ubatili, kukimbiza upepo.

10 Chochote ambacho kimekuwapo, tayari kimepewa jina, na mwanadamu anajulikana alivyo; naye hawezi kuzozana na* yule aliye na nguvu zaidi yake. **11** Kadiri maneno* yalivyo mengi, ndivyo ubatili ulivyo mwingi; nayo humnufaishaje mwanadamu? **12** Ni nani anayejua ni jambo gani lililo bora kwa mwanadamu kufanya maishani katika siku chache za maisha yake ya ubatili, anazotumia kama kiviuli?^c Kwa maana ni nani anayeweza kumwambia mwanadamu yatakayotukia chini ya jua baada ya kifo chake?

7 Jina zuri* ni bora kuliko mafuta mazuri,^d na siku ya kufa ni bora kuliko siku ya kuzaliwa. **2** Ni afadhali kwenda katika nyumba yenye maombolezo kuliko kwenda katika nyumba yenye karamu,^e kwa sababu huo ndio mwisho wa kila mwanadamu, na walio hai wanapaswa kuweka moyoni jambo hilo. **3** Ni afadhali huzuni kuliko

6:7 *Au "nafsi." 6:8 *Tnn., "kuteembea mbele ya walio hai." 6:9 *Tnn., "kutangatanga kwa nafsi." 6:10 *Au "kujitetea mbele ya." 6:11 *Au labda, "mambo." 7:1 *Au "Sifa nzuri." Tnn., "Kuwa na jina."

kicheko,^a kwa maana uso wenyewe huzuni huboresha moyo.^b **4** Moyo wa mwenye hekima uko katika nyumba yenyewe maombolezo, lakini moyo wa mpumbavu uko katika nyumba yenye nderemo.*^c

5 Ni afadhali kusikiliza kario ipio la mtu mwenye hekima^d kuliko kusikiliza wimbo wa wajinga. **6** Kwa maana kicheko cha mjinga ni kama mlio wa miiba inayoteketea chini ya chungu;^e na hili pia ni ubatili. **7** Lakini ukandamizaji unaweza kumfanya mtu mwenye hekima ashikwe na wazimu, na rushwa huopotisha moyo.^f

8 Ni afadhali mwisho wa jambo kuliko mwanzo wake. Ni bora kuwa na subira kuliko kuwa na roho ya kiburi.^g **9** Usikasirike haraka,^{*h} kwa maana hasira hukaa katika kifua cha wajinga.^{†i}

10 Usiulize: “Mbona siku za zamani zilikuwa bora kuliko hizi?” kwa maana hukuuliza hivyo kwa hekima.^j

11 Hekima pamoja na urithi ni jambo jema na huwanufai sha wale wanaoona mwanga wa mchana.* **12** Kwa maana hekima ni ulinzi^k kama pesa zilivyo ulinzi,^l lakini hii ndiyo faida ya ujuzi: Hekima humhifadhi hai yule aliye nayo.^m

13 Tafakari kazi ya Mungu wa kweli, kwa maana ni nani anayeweza kunyoosha kitu ambacho amekipinda?ⁿ

14 Siku iliyo njema, tafakari wema huu,^o lakini katika siku ya taabu,* zingatia kwamba Mungu ameifanya hii na hiyo nyingine,^p ili wanadamu wasi-

SURA YA 7

a Zb 119:71

Lu 6:21

b 2Ko 7:10

Ebr 12:11

c 1Sa 25:36

Met 21:17

d Zb 141:5

Met 15:31

e Mhu 2:2

f Kut 23:8

Kum 16:19

1Sa 8:1-3

Met 17:23

g Met 13:10

Yak 5:10

1Pe 5:5

h Met 16:32

Yak 1:19

i Mwa 4:5

Est 5:9

Met 14:17, 29

Met 29:11

j Lu 9:62

k Met 4:5, 6

l Met 10:15

m Met 3:13, 18

Met 8:35

Met 9:11

n Ayu 9:12

Isa 14:27

o Yak 5:13

p Ayu 2:10

Isa 45:7

Safu ya 2

a Met 27:1

Mhu 9:11

Yak 4:13, 14

b Zb 39:5

c Mwa 4:8

1Sa 22:18

d Ayu 21:7

Zb 73:12

e Isa 65:5

Mt 6:1

Ro 10:3

Ro 14:10

f Met 3:7

Ro 12:3

g Met 16:18

h Zb 14:1

Met 14:9

i Zb 55:23

Met 10:27

j Flp 4:5

k Met 21:22

Met 24:5

l 2Nya 6:36

Zb 51:5

Ro 3:23

1Yo 1:8

m 1Sa 24:9

n Yak 3:2, 8, 9

o Zb 36:6

Zb 139:6

Isa 55:9

Ro 11:33

weze kuwa na uhakika kuhusu* jambo lolote litakalowapata wakati ujao.^a

15 Katika maisha yangu ya ubatili^b nimeona kila jambo —nimemwona mwadilifu akiangamia katika uadilifu wake^c na mwovu akiishi maisha marefu licha ya uovu wake.^d

16 Usiwe mwadilifu kupita kiasi,^e wala kujifanya mwenye hekima kupita kiasi.^f Kwa nini ujiangamize?^g **17** Usiwe mwovu kupita kiasi, wala kuwa mjinga.^h Kwa nini ufe kabla ya wakati wako?ⁱ **18** Ni bora kushika kabisa onyo moja bila kuachilia lingine;^j kwa maana anayemwogopa Mungu atatii yote mawili.

19 Hekima humfanya mtu mwenye hekima awe na nguvu zaidi kuliko wanaume kumi wenye nguvu walio jijini.^k **20** Kwa maana hakuna mtu mwadilifu duniani anayefanya mema sikuzote na hatendi dhambi kamwe.^l

21 Pia, usitie moyoni kila neno linalosemwa na watu;^m la sivyo, huenda ukamsikia mtumishi wako akisema mambo maovu kukuhusu;^{*n} **22** kwa maana unajua vema moyoni mwako kwamba wewe mwenyewe umesema mambo maovu kuwahusu wengine.ⁿ

23 Niliyapima mambo hayo yote kwa hekima, nikasema: “Nitakuwa na hekima.” Lakini ilikuwa mbali nami. **24** Lile ambalo limekuja kuwapo halifikiki nalo ni lenye kina kirefu sana. Ni nani anayeweza kulielewa?^o **25** Niliuongoza moyo wangu kujua na kuchunguza na kutafuta hekima na maana ya mambo, na kuele-

7:14 *Au “kugundua.” 7:21 *Tnn., “akikulaani.”

7:4 *Au “burudani.” 7:9 *Tnn., “Usiwe mwepepi kukasirika rohoni mwako.”
*Au labda, “ni dalili ya mjinga.” 7:11
*Yaani, walio hai. 7:14 *Au “majanga.”

wa uovu wa upumbavu na ujinga wa kuwa wazimu.^a **26** Ki-sha nikagundua hili: Mwanamke ambaye ni kama wavu wa mwindaji anatia uchungu kuliko kifo, ambaye moyo wake ni kama nyavu za kukokotwa, na ambaye mikono yake ni kama minyororo ya gereza. Mtu anayempendeza Mungu wa kweli atamkwepa mwanamke huyo,^b lakini mtenda dhambi hunaswa naye.^c

27 "Tazama, hili ndilo nililogundua," asema mkutani-shaji.^d "Nilichunguza jambo moja baada ya lingine ili nifikie mkataa wangu, **28** lakini jambo nililoendelea* kutafuta, sijalipata. Nimempata mwanamume mmoja^e kati ya elfu moja, lakini sijampata mwanamke miongoni mwao. **29** Hili ndilo jambo pekee nililopata: Mungu wa kweli aliwaumba wanadamu wakiwa wanyoofu,^e lakini wao wenyewe wamejitafutia wapango mingi."^f

8 Ni nani aliye kama mwenye hekima? Ni nani anayejua suluhisho la tatizo? Hekima ya mtu huutia nuru uso wake na kuilainisha sura yake ngumu.

2 Nasema: "Tii maagizo ya mfalme^g kwa sababu ya kiapo chako kwa Mungu.^h **3** Usifanye haraka kuondoka mbele ya mfalme.ⁱ Usitetee jambo lolote baya;^j kwa kuwa anaweza kufanya jambo lolote apendalo, **4** kwa sababu neno la mfalme ni uamuzi wa mwisho;^k ni nani anayeweza kumuuliza: 'Unafanya nini?'"

5 Mtu anayeshika amri hapata madhara,^l na moyo we-

7:28 *Au "ambalo nafsi yangu ilie-ndelea." ^aAu "mwanamume mmoja mnyoofu." **8:1** *Au "maana ya jambo."

SURU YA 7

a Mhu 1:17
Mhu 2:12

b Mwa 39:7-9

c Met 5:3, 14
Met 7:22, 23
Met 22:14

d Mhu 1:1

e Mwa 1:26, 31

f Mwa 3:6
Mwa 6:12
Kum 32:5

SURU YA 8

g Met 24:21, 22
Ro 13:1
Tit 3:1
1Pe 2:13

h 2Sa 5:3

i Mhu 10:4

j 1Fa 1:5, 7
Met 20:2

k 1Fa 2:24, 25

l Ro 13:5
1Pe 3:13

Safu ya 2

a 1Sa 24:12, 13
1Sa 26:8-10
Zb 37:7

b Mhu 3:17

c Zb 89:48

d Kut 1:13, 14
Mik 7:3

e Met 10:7

f Zb 10:4, 6

g 1Sa 2:22, 23

nye hekima utajua wakati unaofaa na utaratibu unao-faa.*^a **6** Kwa maana kila jambo lina wakati wake na utaratibu wake,^{*b} kwa sababu matatizo ya wanadamu ni mengi sana. **7** Kwa kuwa hakuna mtu anayejua litakalotukia, ni nani anayeweza kumwambia jinsi litakavyotukia?

8 Kama vile ambavyo hakuna mtu aliye na nguvu juu ya roho* au anayeweza kuzuia roho, vivyo hivyo hakuna yeyote aliye na nguvu juu ya siku ya kufa.^c Kama vile ambavyo hakuna yeyote anayeruhusiwa kurudi nyumbani wakati wa vita, vivyo hivyo uovu hautawaruhusu wale wanaozoea kuutenda waponyoke.^d

9 Hayo yote nimeyaona, nami nimetafakari moyoni mwangu kila kazi ambayo imefanywa chini ya jua, wakati ambapo mwanadamu amemtawala mwanadamu mwenzake kwa kuumumiza.*^d **10** Nami nikaona waovu wakizikwa, wale waliokuwa wakiingia na kutoka mahali patakatifu, lakini walisahauliwa upesi katika jiji ambalo walitenda hivyo.^e Hili pia ni ubatili.

11 Kwa sababu hukumu dhidi ya tendo ovu haijatekelezwa upesi,^f moyo wa wanadamu hupata ujasiri wa kutenda uovu.^g **12** Ingawa hue-nda mwovu akatenda uovu mara mia moja na bado aishi kwa muda mrefu, hata hivyo ninajua kwamba mambo yatawaendea vyema wale wanaomwogopa Mungu wa

8:5 *Au "hukumu inayofaa." **8:6** *Au "hukumu yake." **8:8** *Au "pumzi, upepo." ^aAu labda, "uovu hauwezi kuwao-koa waovu." **8:9** *Au "kumdhuru; kumletea hasara."

kweli, kwa sababu wanamwogopa.^a **13** Lakini mambo hayatatamwendea vyema mwovu,^b wala hatarefusha siku zake zilizo kama kivuli,^c kwa sababu hamwogopi Mungu.

14 Kuna jambo la ubatili* ambalo hutukia duniani: Kuna watu waadilifu wanaotendewa kana kwamba walikuwa wametenda uovu,^d na kuna watu waovu wanaotendewa kana kwamba walikuwa wametenda uadilifu.^e Nasema kwamba hili pia ni ubatili.

15 Basi nikapendekeza kushangilia,^f kwa sababu hakuna jambo bora kwa mwanaadamu chini ya jua kuliko kula na kunywa na kushangilia; mambo hayo yanapaswa kufuatana naye anapofanya kazi kwa bidii sikuzote za maisha yake,^g ambazo Mungu wa kweli anampa chini ya jua.

16 Nilijitahidi sana ili moyo wangu upate hekima na ili nione shughuli* zote zinazofanywa duniani,^h hata nilikosa usingizi usiku na mchana.[#] **17** Kisha nikatafakari kazi yote ya Mungu wa kweli, nikatambua kwamba wanadamu hawawezi kufahamu kinachotukia chini ya jua.ⁱ Hata wanadamu wakijitahidi kadirigani, hawawezi kuifahamu. Hata wakidai kwamba wana hekima ya kutosha kujua, kwa kweli hawawezi kuifahamu.^j

9 Kwa hiyo nikatia moyoni mambo hayo yote na kufikia mkataa wa kwamba waadilifu na wenye hekima, na pia kazi zao, zimo mikononi mwa Mungu wa kweli.^k Wanadamu hawajui upendo na chuki ili-

8:14 *Au "linalovunja moyo." **8:16** *Au "kazi." #Au labda, "kwamba watu walali mchana wala usiku."

SURA YA 8

a Zb 34:9
Zb 103:13
Zb 112:1
Isa 3:10
2Pe 2:9

b Zb 37:10
Isa 57:21

c Ayu 24:24

d Mhu 7:15

e Zb 37:7
Zb 73:12

f Zb 100:2

g Mhu 2:24
Mhu 3:12, 13

h Mhu 1:13
Mhu 7:25

i Mhu 3:11
Ro 11:33

j Ayu 28:12
Mhu 7:24
Mhu 11:5

SURA YA 9

k Kum 33:3
1Sa 2:9
Zb 37:5

Safu ya 2

a Mhu 5:15

b Mhu 8:10

c Ayu 3:17-19
Mhu 2:15

d Isa 38:19

e Mwa 3:19
Ro 5:12

f Zb 88:10
Zb 115:17
Zb 146:4
Isa 38:18
Yoh 11:11

g Ayu 7:9, 10
Mhu 2:16

h Mhu 9:10

i Kum 12:7
Zb 104:15
Mhu 2:24

j Kum 16:15
Mdo 14:17

k Da 10:2, 3

l Met 5:18

yokuwepo kabla yao. **2** Wote huwa na mwisho uleule,^{*a} waadilifu na waovu,^b watu wema na safi na wale wasio safi, wale wanaotoa dhambi na wale wasiotoa dhambi. Mtu mwema ni sawa na mtenda dhambi; mtu anayeapa ni sawa na yule anayejihadhari kuhusu kuapa. **3** Jambo hili linalohuzunisha hutukia chini ya jua: Kwa kuwa wote wana mwisho uleule,^{*c} moyo wa wanadamu umejaa pia uovu; na kuna wazimu moyoni mwao muda wote wa maisha yao, kisha wanakufa![#]

4 Kuna tumaini kwa yeyote aliye miongoni mwa walio hai, kwa sababu mbwa aliye hai ni afadhali kuliko simba aliyekufa.^d **5** Kwa maana walio hai wanajua* kwamba watakufa,^e lakini waliokufa hawajui jambo lote kamwe,^f wala hawana thawabu[#] tena, kwa sababu kumbukumbu lote kuwahusu limesahuliwa.^g **6** Pia, upendo wao na chuki yao na wivu wao tayari umetoweka, na hawana tena fungu lolote katika mambo yanayofanywa chini ya jua.^h

7 Nenda, ule chakula chako kwa shangwe, na unywe divai yako kwa moyo mchangamfu,ⁱ kwa kuwa tayari Mungu wa kweli amefurahia kazi zako.^j **8** Mavazi yako na yawe meupe daima,^{*} na usikose kupaka kichwa chako mafuta.^k **9** Furahia maisha pamoja na mke wako mpendwa^l sikuzote za maisha yako ya ubatili, ambazo Mungu amekupa chi-

9:2, 3 *Au "hatima ileile." **9:3** #Tnn., "baada ya hilo wanaenda kwa walio-kufa!" **9:5** *Au "wanatambua." #Au "malipo." **9:8** *Yaani, mavazi yanayong'aa yanayoashiria uchangamfu, si mavazi ya maombolezo.

ni ya jua, sikuzote za ubatili wako, kwa maana hilo ndilo fungu lako maishani na katika kazi yako ngumu unayofanya kwa jasho chini ya jua.^a

10 Jambo lolote unalofanya kwa mkono wako, lifanye kwa nguvu zako zote, kwa sababu hakuna kazi wala mipango wala ujuzi wala hekima Kaburini,^{*b} mahali unapokwenda.

11 Nimeona jambo lingine chini ya jua, ya kwamba sikuzote si wenye mbio wanaoshinda mbio, wala wenye nguvu hawashindi vita,^c wala wenye hekima hawapati chakula sikuzote, wala werevu hawawi na utajiri sikuzote,^d wala wenye ujuzi hawafanikiwi sikuzote,^e kwa sababu wakati na matukio yasiyotarajiwa^{*} huwapata wote. **12** Kwa maana mwanadamu hajui wakati wake.^f Kama samaki wavyononasa na wavu mwovu na ndege wavyononasa na mtego, ndivyo wanadamu wavyononasa wakati wa msiba, unapowapata kwa ghafla.

13 Niliona pia jambo hili kuhusu hekima chini ya jua—nalo likanivutia: **14** Kuli kuwa na jiji dogo lenye wanaume wachache; na mfalme mwenye nguvu akaja, akalizingira, na kujenga ukuta mkubwa ili kulishambulia. **15** Mtu fulani maskini lakini mwenye hekima alipatikana katika jiji hilo, naye akaliokoa kwa hekima yake. Lakini hakuna aliyemkumbuka maskini huyo.^g **16** Basi nikajiambia: ‘Hekima ni bora kuliko nguvu;^h hata hivyo hekima ya maskini hudharauliwa, na maneno yake hayasikilizwi.’ⁱ

9:10 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 9:11 *Au “tukio lisilotazamiwa.”

SURA YA 9

a Mhu 5:18

b Zb 115:17
Zb 146:3, 4
Isa 38:18c 1Sa 17:50
Zb 33:16

d Mhu 2:15

e 2Sa 17:23

f Mhu 8:8
Yak 4:13, 14

g Mhu 9:11

h Met 21:22
Met 24:5
Mhu 7:12, 19
Mhu 9:18i Mk 6:3
1Ko 2:8

Safu ya 2

a Yos 22:20
1Ko 5:6
Ebr 12:15

SURA YA 10

b Hes 20:10, 12
2Sa 12:9-11c Met 14:8
Met 17:16

d Met 10:23

e Met 13:16
Met 18:7

f Mhu 8:2, 3

g 1Sa 25:23, 24
Met 25:15h 1Sa 26:21
1Fa 12:13, 14

i Met 30:21-23

j Met 26:27

17 Ni afadhali kusikiliza maneno matulivu ya wenye hekima kuliko kelele za yule anayetawala miongoni mwa wajinga.

18 Hekima ni bora kuliko silaha za vita, lakini mtenda dhambi mmoja tu anaweza kuharibu mambo mengi mazuri.^a

10 Kama nzi waliokufa wavyofanya mafuta ya mtengenezaji wa marashi yanuke na kutoa povu, ndivyo ujinga kidogo unavyozidi hekima na utukufu.^b

2 Moyo wa mwenye hekima humwongoza katika njia inayofaa,^{*} lakini moyo wa mpumbavu humwongoza katika njia isiyofaa.^{†c} **3** Katika njia yoyote ambayo mjinga anatembea, hana busara,^{*d} naye huacha kila mtu ajue kwamba yeye ni mjinga.^e

4 Hasira^{*} ya mtawala ikiwaka dhidi yako, usiondoke mahali pako,^f kwa maana utulivu huzaia dhambi kubwa.^g

5 Kuna jambo linalohuzunisha ambalo nimeona chini ya jua, aina ya kosa linalofanywa na watawala:^h **6** Ujinga huwekwa katika vyeo vingi vya juu, lakini matajiri^{*} hubaki kwenye vyeo vya chini.

7 Nimeona watumishi wakiwa wamepanda farasi lakini wakuu wakitembea kwa miguu kama watumishi tu.ⁱ

8 Anayechimba shimo huenda akaanguka ndani yake;^j na anayebomoa ukuta wa mawe huenda akaumwa na nyoka.

10:2 *Tnn., “uko kwenye mkono wake wa kulia.” [†]Tnn., “uko kwenye mkono wake wa kushoto.” **10:3** *Tnn., “moyo wake umepungukiwa.” **10:4** *Tnn., “Roho, Pumzi.” **10:6** *Au “wanaostahili.”

9 Anayechimbua mawe huenda yakamuumiza, na yule anayepasua magogo huenda yakamuumiza.*

10 Ikiwa kifaa cha chuma hakina makali na mtu hakinoi, atahitaji kutumia nguvu nyingi. Lakini hekima husaidia kuleta mafanikio.

11 Nyoka akiuma kabla hachezeshwa, mtu anayemchezeshwa kwa ustadi* hapati faida yoyote.

12 Maneno yanayotoka kwenye kinywa cha mwenye hekima huleta kibali,^a lakini midomo ya mpumbavu ndiyo inayomwangamiza.^b **13** Maneno ya kwanza yanayotoka katika kinywa chake ni ujinga,^c na maneno yake ya mwisho ni wazimu unaoleta msiba. **14** Lakini mjinga huendelea kuongea.^d

Mwanadamu hajui yatakayotukia; ni nani anayeweza kumwambia yatakayotukia baada yake?^e

15 Kazi ngumu ya mpumbavu humchosha kabisa, kwa sababu hata hajui jinsi atakavyofika jijini.

16 Ole kwa nchi ambayo mfalme wake ni mvulana^f na wakuu wake huanza karamu asubuhi! **17** Yenye furaha ni nchi ambayo mfalme wake ni mwana wa watu mashuhuri na wakuu wake hula wakati unaofaa ili wapate nguvu, si walewe!^g

18 Kwa sababu ya uvivu unaopita kiasi paa hubonyea, na kwa sababu ya mikono milegevu nyumba huvuja.^h

19 Mkate umekusudiwa* kuleta kicheko, na divai hufaa

10:9 *Au labda, "anapaswa kujihadhari nayo." 10:11 *Tnn., "stadi wa ulimi." 10:19 *Au "Chakula kimekusudiwa."

SURA YA 10

a 1Fa 10:6, 8
Zb 37:30
Lu 4:22
Efe 4:29

b Zb 64:2, 8
Met 10:14, 21
Met 14:3

c 1Sa 25:10, 11

d Met 10:19
Met 15:2

e Met 27:1
Mhu 6:12
Yak 4:13, 14

f 2Nya 13:7
2Nya 36:9

g Met 31:4, 5

h Met 21:25
Met 24:33, 34

Safu ya 2

a Zb 104:15
Mhu 9:7

b Mhu 7:12

c Kut 22:28

SURA YA 11

d Met 22:9

e Kum 15:10, 11
Met 19:17
Lu 14:13, 14
Ebr 6:10

f Zb 37:21
Lu 6:38
2Ko 9:7
1Ti 6:18

g Met 20:4

h Zb 139:15

i Ayu 26:14
Zb 40:5
Mhu 8:17
Ro 11:33

j Mhu 9:10
2Ko 9:6
Kol 3:23

k Mhu 5:18
Mhu 8:15

nya maisha yafurahishe;^a lakini pesa ni jawabu la mahitaji yote.^b

20 Usimtukane* mfalme hata katika mawazo yako,^c na usiwatukane matajiri katika chumba chako cha kula; kwa sababu huenda ndege^d akapeleka habari zako,^e au huenda kiumbe mwenye mabawa akarudia lililosemwa.

11 Tupa* mkate wako juu ya maji,^d kwa maana baada ya siku nyingi utaupata tena.^e **2** Wagawie watu saba au hata wanane,^f kwa maana hujui ni msiba gani utakao tokea* duniani.

3 Mawingu yakijaa maji, mvua itanyesha duniani; na mti ukianguka kuelekea kusini au kaskazini, utabaki mahali ulipoanguka.

4 Anayeangalia upepo hatapanda mbegu, na anayetazama mawingu hatavuna.^g

5 Kama usivyojua jinsi roho inavyofanya kazi ndani ya mifupa ya mtoto aliye tumboni mwa mama yake,^h vivyo hivyo hujui kazi ya Mungu wa kweli, anayefanya mambo yote.ⁱ

6 Panda mbegu zako asubuhi na usipumzishie mkono wako mpaka jioni;^j kwa maana hujui ni mbegu gani itakayofanikiwa, hii au ile, au ikiwa zote mbili zitafanikiwa.

7 Mwangaza ni mtamu, na ni vizuri mako yaone jua.

8 Kwa maana ikiwa mwanadamu ataishi miaka mingi, na aifurahie yote.^k Lakini anapaswa kukumbuka kwamba hue-

10:20 *Au "Usimlaani." #Au labda, "kitandani mwako." ^Tnn., "kiumbe anayeruka angani." *Tnn., "sauti yako." 11:1 *Au "Sambaza." 11:2 *Au "janga gani litakalotokea."

nda siku za giza zikawa nyingi; yote yatakayokuja ni ubatili.^a

9 Shangilia, ewe kijana, wakati ungali kijana, na moyo wako ushangilie siku za ujana wako. Fuata njia za moyo wako na uende mahali ambapo macho yako yanakuongoza; lakini ujue kwamba Mungu wa kweli atakuhukumu* kwa sababu ya mambo hayo yote.^b

10 Kwa hiyo ondoa mahangaioko moyoni mwako, na ujepushe na mambo yanayodhuru mwili wako, kwa maana ujana na upeo wa maisha ni ubatili.^c

12 Basi, mkumbuke Muumba wako Mkuu katika siku za ujana wako,^d kabla hazijaja siku za taabu*^e wala haijafika miaka utakaposema: "Siifurahii"; **2** kabla jua na mwangaza na mwezi na nyota hazijawa na giza,^f na mawingu kurudi baada ya* mvua kubwa; **3** siku ambayo walinzi* wa nyumba wanatetemeka,^g na wanaume wenye nguvu wanainama, na wanawake wanaacha kusaga kwa sababu wamekuwa wachache, na mabibi wanaochungulia madirishani wanaona giza;^g **4** milango inayoelekea barabarani inapokuwa imefungwa, sauti ya jiwe la kusagia inapopungua, mtu anapoamshwa na mlio wa ndege, na mabinti wote wanaoimba wanapofifia.^h **5** Pia, mtu anapoogopa sehemu zilizo juu, na vitisho vinapokuwa barabarani. Na mti wa mlozi unapochanua,ⁱ na pilipili inapopasuka, kwa sababu mwanadamu anatembea

11:9 *Au "atakufanya uwajibike." 12:1 *Au "msiba." 12:2 *Au labda, "yakiwa na." 12:3 *Au "watunzaji." *Au "wanatikisika."

SURA YA 11

a Mhu 12:1

b Mhu 3:17
Mhu 12:14
Ro 2:6c Zb 25:7
2Ti 2:22

SURA YA 12

d Zb 71:17
Zb 148:7, 12
Lu 2:48, 49
2Ti 3:15

e Zb 90:10

f 1Sa 4:15

g Mwa 48:10

h 2Sa 19:34, 35

i Met 16:31

Safu ya 2

a Ayu 30:23
Mhu 9:10

b Mwa 50:7, 10

c Mwa 3:19
Zb 146:4d Mwa 2:7
Ayu 27:3
Ayu 34:14, 15
Zb 104:29
Isa 42:5

e 1Fa 8:1

f Mhu 1:2, 14

g 1Fa 10:1, 3
1Fa 10:6, 8h 1Fa 4:29, 32
Met 1:1i Met 16:24
Met 25:11j Mdo 2:37
Ebr 4:12

k Mhu 1:18

l Ayu 28:28
Zb 111:10
Met 1:7

m 1Yo 5:3

n Kum 6:1, 2
Kum 10:12o Zb 62:12
Mhu 11:9
Mt 12:36, 37
Mdo 17:31
2Ko 5:10
1Ti 5:24

kwenda kwenye nyumba yake ya kudumu^a na waombolezaji wanatembeatembea barabarani;^b **6** kabla kamba ya fedha haijaondolewa, na bakuli la dhahabu kuvunjwa, na mtungi ulio kwenye chemchemi kuvunjika, na gurudumu la tangi la maji kuvunjwa. **7** Kisha mavumbi hurudi ardhini,^c mahali yalikotoka, na roho* hurudi kwa Mungu wa kweli aliyewapa wanadamu.^d

8 "Ubatili mkubwa kupita wote!" asema mkutanishaji.^e "Kila kitu ni ubatili."^f

9 Mkutanishaji hakupata tu hekima bali pia aliendelea kuwafundisha watu mambo aliyojua,^g naye alitafakari na kufanya uchunguzi kamili ili atunge* methali nyingi.^h **10** Mkutanishaji alijitahidi kutafuta maneno yanayopendezaⁱ na kuandika maneno sahihi ya kweli.

11 Maneno ya wenye hekima ni kama michokoo ya kuongozea ng'ombe,^j na misemo yao iliyokusanywa ni kama misumari iliyopigiliwa ikawa imara; yametolewa na mchungaji mmoja. **12** Kuhusu jambo lingine lolote zaidi ya hayo, mwanangu, jihadhari: Hakuna mwisho wa kutunga vitabu vingi, na kuvisoma sana huuchosha sana mwili.^k

13 Huu ndio umalizio, baada ya mambo yote kusikiwa: Mwogope Mungu wa kweli^l na ushike amri zake,^m kwa maana huu ndio wajibu wote wa mwanadamu.ⁿ **14** Kwa maana Mungu wa kweli atahukumu kila tendo, kutia ndani kila jambo lililofichwa, kuwa jema au baya.^o

12:7 *Au "nguvu ya uhai." 12:9 *Au "apange kwa utaratibu."

WIMBO WA SULEMANI

YALIYOMO

MSICHANA MSHULAMI AKIWA KWENYE KAMBI
YA MFALME SULEMANI (1:1-3:5)

- 1 Wimbo wa nyimbo (1)
Msichana (2-7)
Mabinti wa Yerusalemu (8)
Mfalme (9-11)
“Tutakutengenezea mapambo ya dhahabu” (11)
Msichana (12-14)
‘Mpenzi wangu ni kama mfuko wa manukato ya manemane’ (13)
Mchungaji (15)
“Wewe ni mrembo, mpenzi wangu”
Msichana (16, 17)
“Wewe ni mrembo, mpenzi wangu” (16)
- 2 Msichana (1)
“Mimi ni ua la zafarani”
Mchungaji (2)
‘Mpenzi wangu ni kama yungiyungi’
Msichana (3-14)
‘Msiamshe upendo mpaka utakapoamka wenyewe’ (7)
Maneno ya mchungaji (10b-14)
“Mrembo wangu, njoo twende zetu” (10b, 13)
Ndugu za msichana (15)
“Tukamatieni mbweha”
Msichana (16, 17)
“Mpenzi wangu ni wangu mimi, na mimi ni wake” (16)
- 3 Msichana (1-5)
‘Usiku, nilimtafuta ninayempenda’ (1)

MSHULAMI AKIWA YERUSALEMU (3:6-8:4)

- 3 Mabinti wa Sayuni (6-11)
Maelezo kuhusu msafara wa Sulemani
- 4 Mchungaji (1-5)
“Wewe ni mrembo, mpenzi wangu” (1)
Msichana (6)
Mchungaji (7-16a)
‘Umeuteka moyo wangu, bibi harus wangu’ (9)
Msichana (16b)

- 5 Mchungaji (1a)
Wanawake wa Yerusalemu (1b)
‘Leweni mapenzi!’
Msichana (2-8)
Asimulia ndoto yake
Mabinti wa Yerusalemu (9)
“Mpenzi wako ni bora kuliko wapenzi wengine wote jinsi gani?”
Msichana (10-16)
“Anavutia zaidi miongoni mwa wanaume elfu kumi” (10)
- 6 Mabinti wa Yerusalemu (1)
Msichana (2, 3)
“Mimi ni wa mpenzi wangu, na mpenzi wangu ni wangu mimi” (3)
Mfalme (4-10)
“Wewe ni mrembo kama Tirsa” (4)
Maneno ya wanawake (10)
Msichana (11, 12)
Mfalme (na wengine) (13a)
Msichana (13b)
Mfalme (na wengine) (13c)
- 7 Mfalme (1-9a)
“Unapendeza sana, ewe msichana mpendwa” (6)
Msichana (9b-13)
“Mimi ni wa mpenzi wangu, naye ananitamani” (10)
- 8 Msichana (1-4)
“Laiti ungekuwa kama ndugu yangu” (1)

MSHULAMI ARUDI, ATHIBITISHA USHIKAMANIFU
WAKE (8:5-14)

- 8 Ndugu za msichana (5a)
‘Ni nani huyu anayemwegemea mpenzi wake?’
Msichana (5b-7)
“Upendo una nguvu kama kifo” (6)
Ndugu za msichana (8, 9)
“Akiwa ukuta, . . . lakini akiwa mlango, . . .” (9)
Msichana (10-12)
“Mimi ni ukuta” (10)
Mchungaji (13)
‘Acha nisikie sauti yako’
Msichana (14)
“Kimbia mbio kama swala”

1 Wimbo wa nyimbo,* ambao ni wa Sulemani:^a

2 “Unibusu* kwa mabusu ya kinywa chako,

Kwa maana maonyesho yako ya mapenzi ni bora kuliko divai.^b

3 Manukato ya mafuta yako mbalimbali yana-
pendeza.^c

Jina lako ni kama mafuta yaliyomiminwa yenye manukato.^d

Ndiyo sababu wasichana wanakupenda.

4 Nichukue;* acha tuki-
mbie.

Mfalme amenileta katika vyumba vyake vya ndani!

Na tufurahi na kukusha-
ngilia.

Na tusifu* maonyesho yako ya mapenzi kuliko divai.

Wana[^] haki ya kukupenda.

5 Mimi ni mweusi, lakini napendeza, enyi mabinti wa Yerusalemu,

Kama mahema ya Kedari,^e kama vitambaa vya mahema^f ya Sulemani.

6 Msinikodolee macho kwa sababu mimi ni mweusi,

Kwa sababu jua limenichoma.

Wana wa mama yangu walinikasirikia;

Walinifanya kuwa mlinzi wa mashamba ya miza-
bibu,

Lakini sikulinda shamba langu mwenyewe la mizabibu.

1:1 *Au “Wimbo ulio bora.” 1:2 *Anayeonea ni msichana. 1:4 *Tnn., “Nivute nikufuate.” *Au “tusimulie.”
[^]Yaani, wale wasichana.

SURA YA 1

a 1Fa 4:29, 32

b Wim 4:10

c Met 27:9
Mhu 9:8
Wim 5:5

d Mhu 7:1

e Zb 120:5
Eze 27:21

f Kut 36:14

Safu ya 2

a Wim 6:3

b 1Fa 10:28
2Nya 1:16, 17
Wim 6:4

c Wim 4:13, 14

d Kut 30:23, 25
Est 2:12
Zb 45:8
Wim 4:6
Wim 5:13

e Wim 4:13

WIMBO WA SULEMANI 1:1-14

7 Niambie, wewe ninayekupenda* sana,

Mahali unapochunga mifugo yako,^a

Mahali unapoipumzisha wakati wa adhuhuri.

Kwa nini niwe kama mwanamke aliyefuni-
kwa shela[#]

Kati ya makundi ya wenzako?”

8 “Ikiwa hujui, ewe mwanamke mrembo kuliko wote,

Nenda ufuata nyayo za mifugo

Na uchunge wanambuzi wako karibu na mahema ya wachungaji.”

9 “Ewe mpenzi wangu, nakufananisha na farasi jike* kati ya magari ya Farao.^b

10 Mashavu yako yanavutia kwa mapambo,*
Shingo yako kwa mikufu ya shanga.

11 Tutakutengenezea mapambo* ya dhahabu Yaliyotiwa vifungo vya fedha.”

12 “Mfalme anapokuwa ameteti kwenye meza yake ya mwingo,

Marashi* yangu^c hunukia.

13 Mpenzi wangu ni kama mfuko wa manemane unaonukia manukato^d
Unaokaa usiku kucha kati-
kati ya matiti yangu.

14 Mpenzi wangu kwangu mimi ni kama kishada cha maua ya hina^e

1:7 *Au “ambaye nafsi yangu inakupenda.” *Tnn., “shela ya maombolezo.” 1:9 *Au “farasi jike wangu.” 1:10 *Au labda, “kati ya nywele zilizosukwa.” 1:11 *Au “mapambo ya duara ya kichwani.” 1:12 *Tnn., “Nardo.”

Kati ya mashamba ya mi-zabibu ya En-gedi.”^a

- 15** “Tazama! Wewe ni mrembo, mpenzi wangu.
Tazama! Wewe ni mrembo. Macho yako ni macho ya njiwa.”^b
- 16** “Tazama! Wewe ni mrembo, * mpenzi wangu, na unapendeza.^c
Kitanda chetu kiko kati ya majani mabichi.
- 17** Maboriti ya nyumba yetu * ni mierezi,
Mapau yetu ni miberoshi.
- 2** “Mimi ni ua la zafarani tu la mwambao wa pwani, Yungiyungi la mabondeni.”^d
- 2** “Kama yungiyungi katikati ya miiba
Ndivyo alivyo mpenzi wangu kati ya mabinti.”
- 3** “Kama mtofaa kati ya miti ya msituni,
Ndivyo alivyo mpenzi wangu miongoni mwa wana.
Natamani sana kukaa katika kivuli chake,
Na tunda lake ni tamu kinywani mwangu.
- 4** Alinileta katika nyumba ya karamu, *
Na bendera aliyoweka juu yangu ilikuwa upendo.
- 5** Niburudishe kwa keki za zabibu kavu;^e
Nilishe matofaa,
Kwa maana naugua kwa mapenzi.
- 6** Amenishika shingoni kwa mkono wake wa kushoto,

1:16 *Au “una sura nzuri.” 1:17 *Au “nyumba yetu kubwa.” 2:4 *Tnn., “nyumba ya divai.”

SURA YA 1

a Yos 15:20, 62
1Sa 23:29
2Nya 20:2

b Wim 4:1
Wim 5:2

c Wim 5:10

SURA YA 2

d Wim 2:16

e 1Sa 30:11, 12

Safu ya 2

a Wim 8:3

b 2Sa 2:18

c Wim 3:5
Wim 8:4

d Wim 2:17
Wim 8:14

e Wim 6:11

f Isa 18:5
Yoh 15:2

g Yer 8:7

h Isa 28:4
Nah 3:12

Na mkono wake wa kulia unanikumbatia.^a

- 7** Nawaapisha, enyi mabinti wa Yerusalemu,
Kwa swala^b na paa jike wa porini:
Msijaribu kuamsha au kuchochea upendo ndani yangu mpaka utakapoa-mka wenyewe.^c
- 8** Sauti ya mpenzi wangu!
Tazama! Ndiye yule anakuja,
Akipanda milima, akirukaruka juu ya vilima.
- 9** Mpenzi wangu ni kama swala, kama paa dume mchanga.^d
Yule pale, amesimama nyuma ya ukuta wetu,
Akichungulia madirishani, Akitazama kupitia viunzi vya madirisha.
- 10** Mpenzi wangu anaongea, ananiambia:
‘Inuka, mpenzi wangu, Mrembo wangu, njoo twendende zetu.
- 11** Angalia, majira ya baridi* yamepita.
Mvua zimekwisha na kwenda zake.
- 12** Maua yamechanua nchini,^e
Wakati wa kupunguza matawi umefika,^f
Na wimbo wa njiwa tetere unasikiwa katika nchi yetu.^g
- 13** Mtini unaivisha tini zake za mapema;^h
Mizabibu inachanua na kunukia manukato.
Inuka, mpenzi wangu, njoo.

2:11 *Au “majira ya mvua.”

Mrembo wangu, njoo twe-
nde zetu.

- 14 Ewe njiwa wangu, kwenye
mapango ya miamba,^a
Kwenye mashimo ya mli-
mani,
Acha nikuone na kusikia
sauti yako,^b
Kwa maana sauti yako ina-
vutia na umbo lako lina-
pendeza.”^c

- 15 “Tukamatieni mbweha,
Mbweha wadogo wanaoha-
ribu mashamba ya miza-
bibu,
Kwa maana mashamba
yetu ya mizabibu yame-
chanua.”

- 16 “Mpenzi wangu ni wangu
mimi, na mimi ni wake.^d
Anachunga kondoo^e kati
ya mayungiyungi.^f

- 17 Mpaka upepo uanze kuvu-
ma* na vivuli kukimbia,
Rudi haraka, ewe mpenzi
wangu,
Kama swala^g au paa dume
mchanga^h juu ya milima
inayotutenganisha.[#]

- 3** “Nyakati za usiku nikiwa
kitandani mwangu,
Nilimtafuta ninayempe-
nda.*ⁱ
Nilimtafuta mwanamume
huyo lakini sikumpata.^j
- 2 Nitaamka na kuzunguka
jijini;
Barabarani na katika viwa-
nja vya mji,
Acheni nimtafute ninaye-
mpenda.*
Nilimtafuta mwanamume
huyo, lakini sikumpata.

2:17 *Tnn., “siku ianze kupumua.” # Au
labda, “milima yenye nyufa.” Au “milima
ya Betheri.” 3:1, 2, 4 *Au “yule amba-
ye nafsi yangu inampenda.”

SURA YA 2

a Wim 5:2
Yer 48:28

b Wim 8:13

c Wim 1:5
Wim 6:10

d Wim 7:10

e Wim 1:7

f Wim 2:1
Wim 6:3

g 2Sa 2:18

h Wim 2:9
Wim 8:14

SURA YA 3

i Wim 1:7

j Wim 5:6

Safu ya 2

a Wim 5:7

b Wim 8:2

c Wim 2:7
Wim 8:4

d Kut 30:23, 24
Kut 30:34

e 1Fa 9:22

- 3 Nilikutana na walinzi wa-
liokuwa wakizunguka
jijini.^a

Nikawauliza, ‘Mmemwona
ninayempenda?’*

- 4 Mara tu baada ya kuwa-
pita
Nilimpata ninayempenda.*

Nikamshika na sikumwa-
cha aende

Mpaka nilipomleta ndani
ya nyumba ya mama
yangu,^b

Katika chumba cha ndani
cha aliyezisa.

- 5 Nawaapisha, enyi binti za
Yerusalemu,

Kwa swala na paa jike wa
porini:

Msijaribu kuamsha au ku-
chochea upendo ndani
yangu mpaka utakapoa-
mka wenyewe.”^c

- 6 “Ni nini hiki kinachokuja
kutoka nyikani kama
nguzo za moshi,

Kilicho na manukato ya
manemane na ubani,

Na manukato yote ya
ungaunga yanayouzwa
na wafanyabiashara?”^d

- 7 “Tazameni! Ni kochi la Su-
lemanu.

Wanaume sitini mashujaa
wanalizinguka,

Miongoni mwa wanaume
mashujaa wa Israeli,^e

- 8 Wote wamejihami kwa
upanga,

Wote wamezoezwa kwa aji-
li ya vita,

Kila mmoja wao ana upa-
nga kiunoni

Ili akabiliane na mambo
yanayotisha wakati wa
usiku.”

3:3 *Au “yule ambaye nafsi yangu ina-
mpenda?”

- 9 “Ni kochi la kifahari* la Mfalme Sulemani Alilojitengenezea kwa mbao za Lebanoni.^a
- 10 Alitengeneza nguzo zake kwa fedha, Viegemeo vyake kwa dhababu. Kiti chake kwa sufu ya zambarau; Sehemu yake ya ndani ilipambwa kwa upendo Na mabinti wa Yerusalemu.”
- 11 “Tokeni nje, enyi binti za Sayuni, Mtazameni Mfalme Sulemani Amevaa taji la harusis* ambalo mama yake^b alimtengenezea Siku yake ya harusis, Siku ambayo moyo wake ulishangilia.”
- 4 “Tazama! Wewe ni mrembo, mpenzi wangu. Tazama! Wewe ni mrembo. Macho yako ni macho ya njiwa nyuma ya shela yako. Nywele zako ni kama kundi la mbuzi Washukao chini kwenye milima ya Gileadi.^c
- 2 Meno yako ni kama kundi la kondoo waliokatwa manyoya sasa hivi Ambao wametoka kuoshwa, Wote wamezaa mapacha, Na hakuna yeyote aliyepoteza watoto wake.
- 3 Midomo yako ni kama uzi mwekundu,

3:9 *Kochi lililofunikwa ambalo lilitumiwa kuwabeba watu mashuhuri. 3:11 *Au “shada; koja la maua.”

SURA YA 3

a 1Fa 5:8, 9

b 2Sa 12:24
Met 4:3

SURA YA 4

c Hes 32:1
Kum 3:12
Wim 6:5-7

Safu ya 2

a Wim 1:10

b Ne 3:25
Wim 7:4c 2Sa 8:7
2Fa 11:10

d Wim 7:3

e Mhu 2:5

f Wim 4:1

g Kum 3:25

h Kum 3:8, 9
Zb 133:3

i Met 5:18, 19

Na maneno yako yanapendeza.

Kama kipande cha komamanga

Ndivyo yalivyo mashavyako nyuma ya shela yako.

- 4 Shingo yako^a ni kama mnara wa Daudi,^b Uliojengwa kwa safu za mawe

Na ngao elfu zimetundi kwa juu yake,

Ngao zote za mviringo za wanaume mashujaa.^c

- 5 Matiti yako mawili ni kama paa wawili wachanga,

Mapacha wa paa,^d

Wanaolisha kwenye mayungungi.”

- 6 “Mpaka upepo uanze kuvuma* na vivuli kukimbia,

Nitakwenda zangu kwenye mlima wa manemane

Na kwenye kilima cha ubani.”^e

- 7 “Wewe ni mrembo kabisa, mpenzi wangu,^f

Huna kasoro yoyote.

- 8 Njoo, bibi harusis wangu, tuondoke Lebanoni,

Njoo tuondoke Lebanoni.^g

Shuka kutoka kilele cha Amana,*

Kutoka kilele cha Seniri, kilele cha Hermoni,^h

Kutoka kwenye mapango ya simba, kutoka kwenye milima ya chui.

- 9 Umeuteka moyo wangu,ⁱ dada yangu, bibi harusis wangu,

4:6 *Tnn., “siku ianze kupumua.” 4:8 *Au “Milima iliyoyanguya ya milima ya Lebanoni.”

Umeuteka moyo wangu
kwa kunitupia jicho
mara moja tu,
Kwa kidani kimoja cha
mkufu wako.

- 10** Maonyesho yako ya upe-
ndo yanavutia kwelikwe-
li,^a dada yangu, bibi
harusi wangu!

Maonyesho yako ya upe-
ndo ni bora zaidi kuliko
divai,^b

Na manukato ya marashi
yako yananukia kuliko
kiungo chochote!^c

- 11** Midomo yako, bibi harusi
wangu, inadondosha
asali ya sega.^d

Chini ya ulimi wako kuna
asali na maziwa,^e

Na manukato ya mavazi
yako ni kama manukato
ya Lebanoni.

- 12** Dada yangu, bibi harusi
wangu, ni kama bustani
iliyofungwa,
Bustani iliyofungwa,
chemchemi iliyofunikwa
kabisa.

- 13** Machipukizi* yako ni
paradiso[#] ya makoma-
manga

Yenye matunda bora kabi-
sa, mimea ya hina na ya
nardo,

- 14** Nardo^f na zafarani, kane*^g
na mdalasini,^h

Iliyo na miti ya kila aina
ya ubani, manemane, na
udi,ⁱ

Pamoja na marashi yote
yaliyo bora kabisa.^j

- 15** Wewe ni chemchemi ya
bustani, kisima cha maji
safi,

4:13 *Au labda, "Ngozi." #Au "busta-
ni." 4:14 *Utete wenyewe harufu nzuri.

SURA YA 4

a Wim 7:12

b Wim 1:2, 4

c Est 2:12
Wim 1:12

d Met 16:24

e Wim 5:1

f Yoh 12:3

g Isa 43:24

h Met 7:17

i Zb 45:8

j Kut 30:23, 24
Kut 30:34
Eze 27:2, 22

Safu ya 2

a Yer 18:14

SURA YA 5

b Wim 4:16

c Wim 4:13, 14

d Wim 4:11

e Wim 1:2

f Wim 3:1

g Lu 2:8

Na vijito vinavyotiririka
kutoka Lebanoni.^a

- 16** Amka, ewe upepo wa kas-
kazini;

Ingia, ewe upepo wa ku-
sini.

Pumueni* kwenye bustani
yangu.

Manukato yake na yae-
nee."

"Mpenzi wangu na aje
kwenye bustani yake

Ale matunda yake yaliyo
bora kabisa."

- 5** "Nimeingia katika bustani
yangu,^b

Ewe dada yangu, bibi ha-
rusi wangu.

Nimekusanya manemane
yangu na viungo* vya-
ngu.^c

Nimekula sega langu na
asali yangu;

Nimekunywa divai yangu
na maziwa yangu."^d

"Kuleni, rafiki zangu wa-
pendwa!

Kunyweni, mlewe maonye-
sho ya upendo!"^e

- 2** "Nimelala usingizi, lakini
moyo wangu uko macho.^f

Ndiyo hiyo sauti ya mpe-
nzi wangu akipiga hodi!

'Nifungulie, ewe dada ya-
ngu, mpenzi wangu,

Njiwa wangu, mpenzi wa-
ngu asiye na kasoro!

Kwa maana kichwa changu
Mashungi ya nywele zangu

yamejaa unyevu wa
usiku.^g

- 3** "Nimevua kanzu yangu.
Ni lazima niivae tena?

4:16 *Au "Vumeni taratibu." 5:1 *Yaa-
ni, vikolezo.

- Nimeosha miguu yangu.
Ni lazima niichafue tena?
- 4** Mpenzi wangu aliondoa mkono wake kwenye tundu la mlango, Hisia zangu kumwelekea zikasisimka.
- 5** Niliinuka ili nimfungulie mpenzi wangu; Mikono yangu ikadondosha manemane, Na vidole vyangu manemane ya maji, Ikadondoka kwenye vitasa vya mlango.
- 6** Nilimfungulia mpenzi wangu, Lakini mpenzi wangu alikuwa ameondoka, alikuwa ameenda zake. Nilitamauka* alipoenda. Nilimtafuta, lakini sikumpata.^a Nikamwita, lakini hakuitika.
- 7** Nilikutana na walenzi waliokuwa wakizunguka jijini. Wakanipiga na kunijeruhi. Walenzi wa kuta wakanivua mtandio wangu.*
- 8** Nawaapisha, enyi binti za Yerusalemu: Mkipata mpenzi wangu, Mwambieni naugua kwa mapenzi.”
- 9** “Mpenzi wako ni bora kuliko wapenzi wengine wote jinsi gani, Ewe mwanamke mrembo kuliko wote? Mpenzi wako ni bora kuliko mpenzi mwingine yeyote jinsi gani, Hivi kwamba unatuapisha hivyo?”

5:6 *Au “Nafsi yangu ilizimia.” 5:7 *Au “shela yangu.”

SURA YA 5

a Wim 3:1, 3

Safu ya 2

a Wim 6:2

b Wim 1:13

c Zb 92:12

d Wim 2:3

- 10** “Mpenzi wangu anang’aa tena ni mwekundu; Anavutia zaidi miongoni mwa wanaume elfu kumi.
- 11** Kichwa chake ni dhahabu, dhahabu bora zaidi. Mashungi ya nywele zake ni kama majani ya mte-nde yanayotikisika.* Nywele zake ni nyeusi kama kunguru.
- 12** Macho yake ni kama njiwa kando ya vijito vya maji, Wanaooga ndani ya maziwa, Wakiwa wameketi kando ya dimbwi lililojaa maji.
- 13** Mashavu yake ni kama kitalu cha viungo,^a Vilima vya mimea yenye manukato. Midomo yake ni mayungiyungi, yanayodondosha manemane ya maji.^b
- 14** Mikono yake ni fito za dhahabu, zilizopambwa kwa krisolito. Tumbo lake ni pembe ya tembo iliyong’arishwa na kufunikwa kwa yakuti.
- 15** Miguu yake ni nguzo za marumaru zilizowekwa kwenye vikalio vya dhahabu bora zaidi. Sura yake ni kama Lebanoni, kama mierezi isiyoni na kifani.^c
- 16** Kinywa chake* ni utamu mtupu, Na kila kitu kumhusu kinatamanika.^d Huyu ndiye mpenzi wangu, huyu ndiye mpendwa wangu, enyi binti za Yerusalemu.”

5:11 *Au labda, “vishada vya tende.”

5:16 *Tnn., “Kaakaa lake.”

- 6** “Mpenzi wako ameenda wapi,
Ewe mwanamke mrembo kuliko wote?
Mpenzi wako amegeuka na kufuata njia gani?
Acha tukamtafute pamoja nawe.”
- 2** “Mpenzi wangu ameshuka kwenda kwenye bustani yake,
Kwenye kitalu cha mimea ya viungo,
Kuchunga kondoo kwenye bustani
Na kuchuma mayungiyungi.^a”
- 3** Mimi ni wa mpenzi wangu,
Na mpenzi wangu ni wangu mimi.^b
Anachunga kondoo kati ya mayungiyungi.”^c
- 4** “Wewe ni mrembo, kama Tirsa,^{*d} mpenzi wangu,^e
Unapendeza kama Yerusalemu,^f
Unavutia sana kama majeshi yaliyokusanyika kuzunguka bendera zao.^g”
- 5** Usinitazame,^h
Ukinitazama nahangaika.
Nywele zako ni kama kundi la mbuzi
Linaloshuka kwenye mitemremko ya Gileadi.ⁱ”
- 6** Meno yako ni kama kundi la kondoo
Ambao wametoka kuoshwa,
Wote wamezaa mapacha,
Na hakuna yeyote aliyepoteza watoto wake.
- 7** Kama kipande cha komamanga
Ndiyoy yalivyo mashavu

6:4 *Au “Jiji Linalopendeza.”

SURA YA 6

a Wim 1:7
Wim 2:16

b Wim 7:10

c Wim 2:16

d 1Fa 14:17
1Fa 15:33

e Wim 1:9

f Zb 48:2

g Wim 6:10

h Wim 1:15
Wim 4:9
Wim 7:4

i Wim 4:1-3

Safu ya 2

a 1Fa 11:1

b Wim 2:14

c Wim 6:4

d Mhu 2:5

yako nyuma ya shela yako.

- 8** Hata kukiwa na malkia 60
Na masuria 80
Na wasichana wasiohesabika.^a
- 9** Lakini kuna mmoja tu ambaye ni njiwa wangu,^b mpenzi wangu asiye na kasoro.
Binti pekee kwa mama yake.
Yeye ni kipenzi cha mama yake.*
Mabinti wanapomwona, humtangaza kuwa mwenye furaha;
Malkia na masuria humsifu.
- 10** ‘Ni mwanamke gani anayeng’aa* kama mapambazuko,
Mrembo kama mwezi mpevu,
Aliye mwangavu kama nuru ya jua,
Mwenye kuvutia sana kama majeshi yaliyokusanyika kuzunguka bendera zao?’^{*c}
- 11** “Nilishuka kwenye bustani ya miti yenye kokwa^d
Ili nione machipukizi bondoni,
Nione ikiwa mzabibu umechipua
Ikiwa mikomamanga imechanua.
- 12** Bila kutarajia,
Tamaa yangu ilinifikisha
Kwenye magari ya watu wangu waungwana.”^{*e}
- 13** “Rudi, rudi, ewe Mshulami!
- 6:9 *Tnn., “ndiye aliye safi sana kwa yule aliyemzaa.” 6:10 *Tnn., “anayetazama chini.” 6:12 *Au “watu wangu walio tayari kusaidia.”

Rudi, rudi,
Ili tukutazame!"
"Kwa nini mnamkodolea
macho Mshulami?"^a
"Yeye ni kama dansi ya ka-
mbi mbili!"^{*}

- 7** "Miguu yako inapendeza
kwelikweli katika viatu
vyako,
Ewe binti unayeheshimika!
Umbo la mapaja yako ni
kama mapambo,
Kazi ya mikono ya fundi.
2 Kitovu chako ni bakuli la
mviringo.
Kisikose kamwe divai iliyo-
tiwa vikolezo.
Tumbo lako ni rundo la
ngano,
Lililozungukwa na mayu-
ngiyungi.
3 Matiti yako mawili ni
kama paa wawili wa-
changa,
Mapacha wa paa.^b
4 Shingo yako^c ni kama
mnara wa pembe ya
tembo.^d
Macho yako^e ni kama vidi-
mbwi kule Heshboni,^f
Karibu na lango la Bath-
rabimu.
Pua yako ni kama mnara
wa Lebanoni,
Unaoelekea Damasko.
5 Kichwa chako kinakuvika
taji kama Karmeli,^g
Na mashungi ya nywele
zako^{*h} ni kama sufu ya
zambarau.ⁱ
Mfalme ameduwazwa[#] na
nywele zako ndefu.
6 Wewe ni mrembo kweli-
kweli, nawe unapendeza
sana,

6:13 *Au "dansi ya Mahanaimu." 7:5
*Tnn., "kichwa chako." #Au "ame-
tekwa."

SURA YA 6

a Wim 1:6

SURA YA 7

b Wim 4:5

c Wim 1:10

d Wim 4:4

e Wim 4:1

f Hes 21:25
Yos 21:8, 39

g Isa 35:2

h Wim 6:5

i Est 8:15

Safu ya 2

a Wim 7:3
Wim 8:10b Wim 2:16
Wim 6:3

c Wim 1:14

d Wim 2:13

e Wim 6:11

f Wim 1:2
Wim 4:10

g Mwa 30:14

h Wim 4:16

Ewe msichana mpendwa,
unazidi vyote vinavyope-
ndeza!

- 7** Kimo chako ni kama cha
mtende,
Na matiti yako ni kama vi-
shada vya tende.^a
8 Nilisema, 'Nitapanda juu
ya mtende
Nishike vitawi vyake vye-
nye tende.'
Matiti yako na yawe kama
vishada vya mizabibu,
Na pumzi yako inanukia
kama matofaa,
9 Na kinywa chako^{*} kama
divai bora kabisa."
"Na ishuke taratibu kwa
ajili ya mpenzi wangu,
Itiririke taratibu juu ya mi-
domo ya mpenzi wangu.[#]
10 Mimi ni wa mpenzi
wangu,^b
Naye ananitamani.
11 Njoo, ewe mpenzi wangu,
Twende mashambani;
Twende tukapumzike kati
ya mimea ya hina.^c
12 Tuamke mapema twende
kwenye mashamba ya
mizabibu
Tuone ikiwa mzabibu ume-
chipuka,
Ikiwa maua yamechanua,^d
Ikiwa mikomamanga ime-
chanua.^e
Huko nitakuonyesha upe-
ndo wangu.^f
13 Dudai^g hutoa harufu yake
nzuri;
Kwenye milango yetu kuna
matunda bora ya kila
aina.^h
Mapya na pia ya zamani,
Ewe mpenzi wangu, nime-
kuhifadhia.

7:9 *Tnn., "kaakaa lako." #Tnn., "mido-
mo ya wanaolala usingizi."

- 8** “Laiti ungekuwa kama ndugu yangu, Aliyeniyonya matiti ya mama yangu! Ngingekukuta nje, ngingekubusu.^a Na hakuna mtu angeni-dharau.
- 2** Ngingekuongoza; Ngingekuleta ndani ya nyumba ya mama yangu,^b Aliyenifundisha. Ngingekupa divai iliyotiwa vikolezo unywe, Maji matamu ya makomamanga.
- 3** Angenishika shingoni kwa mkono wake wa kushoto, Na mkono wake wa kulia ungenikumbatia.^c
- 4** “Nawaapisha, enyi binti za Yerusalemu: Msijaribu kuamsha au kuchochea upendo ndani yangu mpaka utakapoa-mka wenyewe.”^d
- 5** “Ni nani huyu anayekuja kutoka nyikani, Akiwa amemwegemea mpenzi wake?” “Chini ya mtofaa nilikua-msha. Hapo ndipo mama yako alipopata uchungu wa kukuzaa. Hapo ndipo mama yako alipokuzaa kwa uchungu.
- 6** Niweke kama muhuri juu ya moyo wako, Kama muhuri juu ya mkonu wako, Kwa maana upendo una nguvu kama kifo,^e

SURA YA 8

a Wim 1:2

b Wim 3:4

c Wim 2:6

d Wim 2:7
Wim 3:5e Yoh 15:13
Efe 5:25
Ufu 12:11

Safu ya 2

a Kum 4:24
1Yo 4:8

b 1Ko 13:8, 13

c Ro 8:38, 39

d Wim 1:6

e Mhu 2:4

WIMBO WA SULEMANI 8:1-11

- Na kama Kaburi,^{*} ujitoaji kamili haukubali kushi-ndwa. Miale yake ni moto mkali, mwali wa Yah.^{#a}
- 7** Maji yenye nguvu hayawezi kuuzima upendo,^b Wala mito haiwezi kuufagilia mbali.^c Kama mtu angejaribu kuuza mali yote nyumbani mwake kwa ajili ya upendo, Mali hiyo ingedharauliwa^{*} kabisa.”
- 8** “Tuna dada mdogo,^d Ambaye hana matiti. Tutamfanyia nini dada yetu Siku atakapoposwa?”
- 9** “Akiwa ukuta, Tutajenga juu yake mnara wa fedha, Lakini akiwa mlango, Tutamziba kwa ubao mpana wa mwerezi.”
- 10** “Mimi ni ukuta, Na matiti yangu ni kama minara. Kwa hiyo machoni pake ni-mekuwa Kama mtu anayepata amani.
- 11** Sulemani alikuwa na shamba la mizabibu^e kule Baal-hamoni. Aliwakabidhi watunzaji shamba hilo la mizabibu. Kila mmoja wao alikuwa akileta vipande elfu moja vya fedha kwa ajili ya matunda yake.

8:6 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. #“Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. **8:7** *Au labda, “Angedharauliwa.”

- 12** Nina shamba langu mwe-nyewe la mizabibu.
Hivyo vipande elfu moja vya fedha ni vyako,
Ee Sulemani,
Na vipande mia mbili ni vya wale wanaotunza matunda ya shamba hilo.”
- 13** “Wewe unayekaa katika bustani,^a

SURA YA 8

a Wim 1:6
Wim 6:11

Safu ya 2

a Wim 2:14

b Wim 2:9, 17

Rafiki zako wanasikiliza sauti yako.
Acha niisikie.”^a

- 14** “Kimbia, mpenzi wangu, Kimbia mbio kama swala^b
Au paa dume mchanga Juu ya milima yenye viungo.”*

8:14 *Au “vikolezo.”

ISAYA

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Baba na wanawe waasi (1-9)
Yehova anachukia ibada ya kidehuri (10-17)
“Tunyooshe mambo kati yetu” (18-20)
Sayuni litakuwa jiji lenye uaminifu tena (21-31)</p> <p>2 Mlima wa Yehova wainuliwa (1-5)
Panga zitakuwa majembe ya plau (4)
Siku ya Yehova itawafedhehesha wenye majivuno (6-22)</p> <p>3 Viongozi wa Yuda wawapotosha watu (1-15)
Mabinti wa Sayuni wanaotongoza wahukumiwa (16-26)</p> <p>4 Wanawake saba kwa mwanamume mmoja (1)
Atakachochipusha Yehova kitakuwa chenye utukufu (2-6)</p> <p>5 Wimbo kuhusu shamba la Yehova la mizabibu (1-7)
Ole kwa shamba la Yehova la mizabibu (8-24)
Hasira ya Mungu dhidi ya watu wake (25-30)</p> <p>6 Maono ya Yehova katika hekalu lake (1-4)
“Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Yehova” (3)
Midomo ya Isaya yasafishwa (5-7)
Isaya atumwa (8-10)</p> | <p>“Mimi hapa! Nitume mimi!” (8)
“Ni mpaka lini, Ee Yehova?” (11-13)</p> <p>7 Ujumbe kwa Mfalme Ahazi (1-9)
Shear-yashubu (3)
Ishara ya Imanueli (10-17)
Matokeo ya kutokuwa waaminifu (18-25)</p> <p>8 Shambulizi linalokuja la Ashuru (1-8)
Maher-shalal-hash-bazi (1-4)
Usiogope—“Mungu yuko pamoja nasi!” (9-17)
Isaya na watoto wake ni kama ishara (18)
Tafuteni habari katika sheria, si kwa roho waovu (19-22)</p> <p>9 Nuru kuu kwa ajili ya nchi ya Galilaya (1-7)
“Mkuu wa Amani” azaliwa (6, 7)
Mkono wa Mungu dhidi ya Israeli (8-21)</p> <p>10 Mkono wa Mungu dhidi ya Israeli (1-4)
Ashuru—Fimbo ya hasira ya Mungu (5-11)
Ashuru kuadhibiwa (12-19)
Watu waliobaki wa Yakobo watarudi (20-27)
Mungu atahukumu Ashuru (28-34)</p> <p>11 Utawala wa uadilifu wa tawi la Yese (1-10)
Mbwamwitu na mwanakondoo watakaa pamoja (6)</p> |
|--|--|

- Ujuzi kumhusu Yehova utajaa duniani (9)
Waliobaki watarudishwa (11-16)
- 12 Wimbo wa shukrani (1-6)
"Yah Yehova ni nguvu zangu" (2)
- 13 Tangazo dhidi ya Babiloni (1-22)
Siku ya Yehova iko karibu! (6)
Wamedi kuangusha Babiloni (17)
Babiloni halitakaliwa kamwe (20)
- 14 Waisraeli wataishi katika nchi yao (1, 2)
Dhihaka dhidi ya mfalme wa Babiloni (3-23)
Anayeng'aa ataanguka kutoka mbinguni (12)
Mkono wa Yehova utamponda Mwashuru (24-27)
Tangazo dhidi ya Ufilisti (28-32)
- 15 Tangazo dhidi ya Moabu (1-9)
- 16 Ujumbe dhidi ya Moabu waendelea (1-14)
- 17 Tangazo dhidi ya Damasko (1-11)
Mataifa yatakemewa na Yehova (12-14)
- 18 Ujumbe dhidi ya Ethiopia (1-7)
- 19 Tangazo dhidi ya Misri (1-15)
Wamisri watamjua Yehova (16-25)
Madhabahu kwa ajili ya Yehova nchini Misri (19)
- 20 Ishara dhidi ya Misri na Ethiopia (1-6)
- 21 Tangazo dhidi ya nyika ya bahari (1-10)
Kulinda kwenye mnara wa mlinzi (8)
"Babiloni ameanguka!" (9)
Tangazo dhidi ya Duma na nchi tambarare ya jangwani (11-17)
"Mlinzi, kuna habari gani za usiku?" (11)
- 22 Tangazo kuhusu Bonde la Maono (1-14)
Eliakimu awa msimamizi badala ya Shebna (15-25)
Kigingi cha mfano (23-25)
- 23 Tangazo dhidi ya Tiro (1-18)
- 24 Yehova ataifanya nchi kuwa tupu (1-23)
Yehova ni Mfalme katika Sayuni (23)
- 25 Baraka nyingi kwa watu wa Mungu (1-12)
Karamu ya Yehova ya divai bora (6)
Kifo hakitakuwepo tena (8)
- 26 Wimbo kuhusu tumaini na wokovu (1-21)
Yah Yehova, Mwamba wa milele (4)
Watu duniani watajifunza uadilifu (9)
- "Wafu wako wataishi" (19)
Ingieni katika vyumba vya ndani mjifiche (20)
- 27 Yehova amua Lewiathani (1)
Wimbo kuhusu Israeli likiwa shamba la mizabibu (2-13)
- 28 Ole kwa walevi wa Efraimu! (1-6)
Makuhani na manabii wa Yuda wapepesuka (7-13)
"Agano na Kifo" (14-22)
Jiwe la pembeni lenye thamani katika Sayuni (16)
Kazi ya Yehova isiyoye ya kawaida (21)
Mfano kuhusu nidhamu ya Yehova yenye hekima (23-29)
- 29 Ole kwa Arieli! (1-16)
Ibada ya midomo tu yashutumiwa (13)
Viziwi watasikia; na vipofu wataona (17-24)
- 30 Msaada wa Misri ni bure kabisa (1-7)
Watu wakataa ujumbe wa kinabii (8-14)
Mtakuwa na nguvu mkiendelea kuwa na tumaini (15-17)
Yehova awaonyesha kibali watu wake (18-26)
Yehova, Mfundishaji Mkuu (20)
"Hii ndiyo njia" (21)
Yehova atatekeleza hukumu dhidi ya Ashuru (27-33)
- 31 Msaada wa kweli unatoka kwa Mungu, hautoki kwa wanadamu (1-9)
Farasi wa Misri ni nyama tu (3)
- 32 Mfalme na wakuu watatawala kwa haki ya kweli (1-8)
Wanawake wanaopuza mambo waonywa (9-14)
Kumiminwa kwa roho kwaleta baraka (15-20)
- 33 Hukumu na tumaini kwa waadilifu (1-24)
Yehova ni Mwamuzi, Mpaji-sheria, na Mfalme (22)
Hakuna atakayesema: "Mimi ni mgonjwa" (24)
- 34 Kisasi cha Yehova dhidi ya mataifa (1-8)
Edomu itafanywa ukiwa (9-17)
- 35 Paradiso yarudishwa (1-7)
Vipofu wataona; viziwi watasikia (5)
Njia ya Utakatifu kwa ajili ya waliokombolewa (8-10)

- 36 Senakeribu ashambulia Yuda (1-3)
Rabshake amdhihaki Yehova (4-22)
- 37 Hezekia atafuta msaada wa Mungu kupitia Isaya (1-7)
Senakeribu atishia Yerusalemu (8-13)
Sala ya Hezekia (14-20)
Isaya apeleka jibu la Mungu (21-35)
Malaika awaua Waashuru 185,000 (36-38)
- 38 Hezekia ashikwa na ugonjwa kisha apona (1-22)
Wimbo wa shukrani (10-20)
- 39 Wajumbe kutoka Babiloni (1-8)
- 40 Faraja kwa watu wa Mungu (1-11)
Sauti nyikani (3-5)
Ukuu wa Mungu (12-31)
Mataifa kama tone kutoka katika ndoo (15)
Mungu hukaa "juu ya duara ya dunia" (22)
Nyota zote huitwa kwa majina (26)
Mungu hachoki kamwe (28)
Wanaomtumaini Yehova watapata nguvu mpya (29-31)
- 41 Mshindi kutoka mashariki (1-7)
Israeli achaguliwa kuwa mtumishi wa Mungu (8-20)
"Rafiki yangu Abrahamu" (8)
Miungu mingine yajaribiwa (21-29)
- 42 Mtumishi wa Mungu na kazi yake (1-9)
'Jina langu ni Yehova' (8)
Wimbo mpya wa kumsifu Yehova (10-17)
Israeli ni kipofu na kiziwi (18-25)
- 43 Yehova awakusanya tena watu wake (1-7)
Miungu yashtakiwa (8-13)
"Ninyi ni mashahidi wangu" (10, 12)
Waachiliwa huru kutoka Babiloni (14-21)
"Tukutane ili tufanye kesi" (22-28)
- 44 Baraka kwa watu waliochaguliwa na Mungu (1-5)
Hakuna Mungu ila Yehova (6-8)
Upumbavu wa sanamu zilizotengenezwa na wanadamu (9-20)
Yehova, Mkombozi wa Israeli (21-23)
Ukombozi kupitia Koreshi (24-28)
- 45 Koreshi atiwa mafuta ili aliteke Babiloni (1-8)
Udongo haupaswi kushindana na Mfinyanzi (9-13)
- Mataifa mengine yatambua Israeli (14-17)
Mungu anategemeka katika uumbaji na katika kufunua mambo (18-25)
Dunia iliumbwa ili ikaliwe (18)
- 46 Sanamu za Babiloni dhidi ya Mungu wa Israeli (1-13)
Yehova atabiri mambo ya wakati ujao (10)
Ndege anayewinda anayetoka mashariki (11)
- 47 Kuanguka kwa Babiloni (1-15)
Wanajimu wafunuliwa (13-15)
- 48 Watu wa Israeli wakemewa na kusafishwa (1-11)
Yehova atachukua hatua dhidi ya Babiloni (12-16a)
Mafundisho ya Mungu ni yenye faida (16b-19)
"Tokeni Babiloni!" (20-22)
- 49 Kazi ya mtumishi wa Yehova (1-12)
Nuru ya mataifa (6)
Faraja kwa Waisraeli (13-26)
- 50 Dhambi za Waisraeli zasababisha matatizo (1-3)
Mtumishi mtiifu wa Yehova (4-11)
Ulimi na sikio la waliofundishwa (4)
- 51 Sayuni larudishwa kuwa kama bustani ya Edeni (1-8)
Faraja kutoka kwa Muumba wa Sayuni mwenye nguvu (9-16)
Kikombe cha ghadhabu ya Yehova (17-23)
- 52 Amka, Ee Sayuni! (1-12)
Miguu ya wale wanaoleta habari njema inapendeza (7)
Walinzwa na Sayuni wapaza sauti kwa pamoja (8)
Wale wanaobeba vyombo vya Yehova lazima wawe safi (11)
Mtumishi wa Yehova atakwezwa (13-15)
Sura iliyoharibika (14)
- 53 Kuteseka, kufa, na kuzikwa kwa mtumishi wa Yehova (1-12)
Adharauliwa na kuepukwa (3)
Abeba magonjwa na maumivu (4)
"Kama kondoo machinjioni" (7)
Abeba dhambi za wengi (12)
- 54 Sayuni aliye tasa atapata wana wengi (1-17)

- Yehova ni mume wa Sayuni (5)
Wana wa Sayuni watafundishwa na Yehova (13)
Silaha dhidi ya Sayuni zitashindwa (17)
- 55 Mwaliko wa kula na kunywa bure (1-5)
Mtafuteni Yehova na neno lake linalotegemeka (6-13)
Njia za Mungu ziko juu kuliko njia za mwanadamu (8, 9)
Neno la Mungu hakika litafanikiwa (10, 11)
- 56 Baraka kwa wageni na matowashi (1-8)
Nyumba ya sala kwa ajili ya wote (7)
Walenzi vipofu, mbwa walio bubu (9-12)
- 57 Mtu mwadilifu na watu washikamanifu waangamia (1, 2)
Ukahaba wa kiroho wa Israeli wafunuliwa (3-13)
Faraja kwa watu wa hali ya chini (14-21)
Waovu ni kama bahari iliyochafuka (20)
Hakuna amani kwa waovu (21)
- 58 Kufunga kwa kweli na kwa uwongo (1-12)
Kushika Sabato kwa furaha (13, 14)
- 59 Dhambi za Waisraeli zawatenga na Mungu (1-8)
Kuungama dhambi (9-15a)
Yehova huingilia kati kwa ajili ya wanaotubu (15b-21)
- 60 Utukufu wa Mungu wang'aa juu ya Sayuni (1-22)
- Kama njiwa kwenye viota vyao (8)
Dhahabu badala ya shaba (17)
Mdogo atakuwa elfu (22)
- 61 Atiwa mafuta ili kutangaza habari njema (1-11)
"Mwaka wa nia njema ya Yehova" (2)
"Miti mikubwa ya uadilifu" (3)
Watu wa nchi nyingine watasaidia (5)
"Makuhani wa Yehova" (6)
- 62 Jina jipya la Sayuni (1-12)
- 63 Kisasi cha Yehova dhidi ya mataifa (1-6)
Upendo mshikamanifu wa Yehova nyakati za zamani (7-14)
Sala ya toba (15-19)
- 64 Sala ya toba yaendelea (1-12)
Yehova "Mfinyanzi wetu" (8)
- 65 Hukumu ya Yehova dhidi ya wanaoabudu sanamu (1-16)
Mungu wa Bahati Njema na Mungu wa Majaliwa (11)
"Watumishi wangu watakula" (13)
Mbingu mpya na dunia mpya (17-25)
Kujunga nyumba; kupanda mashamba ya mizabibu (21)
Hakuna atakayefanya kazi ngumu bure (23)
- 66 Ibada ya kweli na ibada ya uwongo (1-6)
Sayuni na wanawe (7-17)
Watu wakusanyika Yerusalemu ili kuabudu (18-24)

1 Maono ambayo Isaya^{*a} mwana wa Amози aliona kuhusu Yuda na Yerusalemu katika siku za Uzia,^b Yothamu,^c Ahazi,^d na Hezekia,^e wafalme wa Yuda:^f

2 Sikieni, enyi mbingu, na usikilize, ewe dunia,^g
Kwa maana Yehova amesema:
"Nimelea wana wakakua,^h
Lakini wameniasi.ⁱ

1:1 *Maana yake "Wokovu wa Yehova."

SURA YA 1

a 2Nya 32:32

b 2Nya 26:22

Isa 6:1

c 2Nya 27:1, 2

d 2Nya 28:1

e 2Nya 29:1, 2

2Nya 32:20

f Mt 1:9

g Zb 50:4

h Kum 1:31

i Kum 4:25, 26

Eze 20:8

Safu ya 2

a Ho 4:6

b Da 9:11

3 Ng'ombe anamjua vizuri aliyemnuna,
Na punda anajua vizuri hori ya mmiliki wake;
Lakini Israeli hanijui,^{*a}
Watu wangu mwenyewe hawatendi kwa uelewaji."

4 Ole kwa taifa lenye dhambi,^b
Watu waliolemewa na dhambi,

1:3 *Au "hamjui bwana wake."

Uzao wa watu waovu,
watoto waliopotoka!
Wamemwacha Yehova;^a
Wamemvunjia heshima
Mtakatifu wa Israeli;
Wamemgeuzia migongo
yao.

- 5 Ni wapi mtakapopigwa
tena kwa kuwa mnazidi
kuasi?^b

Kichwa chote ni kigonjwa,
Na moyo wote ni mgonjwa.^c

- 6 Kuanzia wayo wa mguu
mpaka kichwani, hakuna
sehemu yenye afya.

Kuna majeraha na michu-
buko na vidonda vilivyo
wazi

—Havijatibiwa* wala ku-
fungwa wala kulainishwa
kwa mafuta.^d

- 7 Nchi yenu ni ukiwa.
Majiji yenu yameteketewa
kwa moto.

Wageni wanaila nchi yenu
mbele ya macho yenu.^e

Ni kama nchi iliyo ukiwa
iliyoharibiwa kabisa na
wageni.^f

- 8 Binti ya Sayuni ameachwa
kama kibanda katika
shamba la mizabibu,

Kama nyumba ya msonge
katika shamba la ma-
tango,

Kama jiji lililozingirwa.^g

- 9 Kama Yehova wa majeshi
hangetuachia waokokaji
wachache,
Tungekuwa kama Sodoma,
Na tungefanana na Go-
mora.^h

- 10 Sikieni neno la Yehova,
enyi madikteta* wa So-
doma.ⁱ

1:6 *Tnn., "Havijafinywa; Havijatum-
liwa." 1:10 *Au "watawala."

SURA YA 1

a Kum 31:16
Yer 2:5

b Yer 5:3

c Ne 9:34, 35
Da 9:8

d Lu 10:34

e Kum 28:33, 63

f 2Fa 18:11

g 2Fa 18:13, 14
Isa 8:7, 8

h Mwa 19:24, 25
Kum 29:22, 23
Ro 9:29

i Mwa 13:13
Isa 3:8, 9

Safu ya 2

a Kum 32:32
Yud 7

b 1Sa 15:22
Met 15:8
Ho 6:6
Mik 6:7

c Kut 29:38

d Law 3:14-16

e Law 17:11

f Law 4:18, 21

g Law 16:5

h Kum 16:16

i Mhu 5:1
Mal 1:8

j Met 21:27
Eze 8:11, 12

k Hes 28:11

l Kut 31:13

m Law 23:2

n Law 19:26

o Met 15:29

p Mt 6:7

q Met 28:9
Isa 59:2
Omb 3:44

r Mik 3:2-4

Sikilizeni sheria* ya Mu-
ngu wetu, enyi watu wa
Gomora.^a

- 11 "Dhabihu zenu nyingi zina
faida gani kwangu?"^b
asema Yehova.

"Nimetosheka na dhabihu
zenu za kuteketezwa za
kondoo dume^c na mafuta
ya wanyama waliolishwa
vizuri,^d

Nami sipendezwi na damu^e
ya ng'ombe dume wacha-
nga^f na wanakondoo na
mbuzi.^g

- 12 Mnapokuja kusimama
mbele zangu,^h

Ni nani ambaye amewata-
ka mfanye hivyo,

Mzikanyage-kanyage nyua
zangu?ⁱ

- 13 Acheni kuleta matoleo
zaidi na nafaka yasiyo na
thamani.

Uvumba wenu unanichu-
kiza.^j

Miezi mipya,^k sabato,^l
kuita makusanyiko^m

—Siwezi kuvumilia matu-
mizi ya nguvu za uchawiⁿ
pamoja na kusanyiko
lenu takatifu.

- 14 Nimechukia* miezi yenu
mipya na sherehe zenu.
Zimekuwa mzigo kwangu;
Nimechoka kuzibeba.

- 15 Na mnaponyoosha mikono
yenu,

Mimi huficha macho
yangu nisiwaone.^o

Ingawa mnatoa sala
nyingi,^p

Mimi sisikilizi;^q

Mikono yenu imejaa
damu.^r

1:10 *Au "mafundisho." 1:14 *Au
"Nafsi yangu imechukia."

- 16** Jiosheni, jisafisheni;^a
Ondoeni matendo yenu
maovu mbele za macho
yangu;
Acheni kutenda mabaya.^b
- 17** Jifunzeni kutenda mema,
tafuteni haki,^c
Mrekebisheni mkandami-
zaji,
Teteeni haki za yatima,
Nanyi mteteeni mjane.”^d
- 18** “Sasa, njooni, na tunyoo-
she mambo kati yetu,”
asema Yehova.^e
“Ingawa dhambi zenu ni
kama rangi nyekundu,
Zitafanywa kuwa nyeupe
kama theluji;^f
Ingawa ni nyekundu kama
kitambaa chekundu,
Zitakuwa kama safu.
- 19** Mkionyesha utayari na ku-
sikiliza,
Mtakula vitu vyema vya
nchi.^g
- 20** Lakini mkikataa na kuasi,
Mtaliwa na upanga,^h
Kwa maana kinywa cha Ye-
hova kimesema hayo.”
- 21** Jinsi mji mwaminifuⁱ ume-
kuwa kahaba!^j
Ulikuwa umejaa haki;^k
Uadilifu ulikuwa ukikaa
ndani yake,^l
Lakini sasa wauaji wana-
kaa ndani yake.^m
- 22** Fedha yako imekuwa taka-
taka,ⁿ
Na pombe yako* imecha-
nganywa na maji.
- 23** Wakuu wako ni wakaidi na
wanashirikiana na wezi.^o
Kila mmoja wao anapenda
rushwa na kutafuta za-
wadi kwa bidii.^p

1:22 *Au “pombe yako ya ngano.”

SURA YA 1

- a Yer 4:14
b Isa 55:7
c Mik 6:8
d Kum 10:18
Yer 22:3
e Mik 6:2
Yak 4:8
f Zb 51:7
Isa 44:22
Mik 7:19
g Kum 28:1, 2
Yoe 2:19
h Law 26:33
Met 29:1
i Zb 48:2
j Yer 2:20
k 2Sa 8:15
IFa 3:28
l 2Nya 19:9, 10
m Mik 3:1-3
Lu 13:34
n Eze 22:18
o Isa 3:14
Mik 3:9-11
p Kut 23:8

Safu ya 2

- a Kut 22:22
Yer 5:28
b Eze 5:13
c Yer 6:29, 30
Yer 9:7
Mal 3:3
d Hes 12:3
1Sa 12:1, 3
Isa 32:1
Eze 34:23
e Isa 62:1
f Yer 31:11
g Eze 20:38
h 1Fa 9:6, 7
i Eze 6:13
j Isa 65:3
Isa 66:17
k Yer 17:5, 6

- Hawawatendei kwa haki
mayatima,
Na kesi ya mjane haiwafi-
kii kamwe.^a
- 24** Kwa hiyo Bwana wa kweli,
Yehova wa majeshi,
Mwenye Nguvu wa Israeli,
anasema:
“Ah! Nitawaondoa wapi-
nzani wangu,
Nami nitaliza kisasi
dhidi ya maadui wangu.^b
- 25** Nitaugeza mkono wangu
dhidi yako,
Nitayeyusha takataka yako
kama kwa sabuni,
Nami nitauondoa uchafu
wako wote.^c
- 26** Nitawarudisha waamuzi
wenu kama mwanzoni
Na washauri wenu kama
awali.^d
Kisha wewe utaitwa Jiji
la Uadilifu, Mji Mwami-
nifu.^e
- 27** Sayuni atakombolewa
kwa haki,^f
Na watu wake wanaorudi,
kwa uadilifu.
- 28** Waasi na watenda dhambi
watavunjwa pamoja,^g
Na wale wanaomwacha Ye-
hova watafikia mwisho
wao.^h
- 29** Kwa maana wataona aibu
kwa sababu ya miti miku-
bwa ambayo mlitamani,ⁱ
Nanyi mtafedheheka kwa
sababu ya bustani*
ambazo mlíchagua.^j
- 30** Kwa maana mtakuwa
kama mti mkubwa
ambao majani yake
yananyauka,^k

1:29 *Inaonekana ni miti na bustani zilizohusiana na ibada ya sanamu.

- Na kama bustani isiyo na maji.
- 31** Mwanamume mwenye nguvu atakuwa kitani,* Na kazi yake itakuwa cheche ya moto; Atateketea motoni pamoja na kazi yake, Na hapatakuwa na yeyote wa kuwazima.”
- 2** Hili ndilo jambo ambalo Isaya mwana wa Amozai aliona katika maono kuhusu Yuda na Yerusalemu:^a
- 2** Katika siku za mwisho,* Mlima wa nyumba ya Yehova Utaimarishwa kabisa juu ya vilele vya milima,^b Nao utainuliwa juu ya vilima, Na mataifa yote yatamimika kwenye mlima huo.^c
- 3** Na watu wa mataifa mengi wataenda na kusema: “Njoooni, twendeni juu kwenye mlima wa Yehova, Kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo.^d Naye atatufundisha njia zake, Nasi tutatembea katika vijia vyake.”^e Kwa maana sheria itatoka* Sayuni, Na neno la Yehova litatoka Yerusalemu.^f
- 4** Atatekeleza hukumu miongoni mwa mataifa Na kunyoosha* mambo kuhusiana na watu wengi. Watafua panga zao ziwe majembe ya plau

1:31 *Nyuzi zinazoshika moto kwa urahisi ambazo zinafanana na kamba. 2:2 *Au “Katika kipindi cha mwisho cha zile siku.” 2:3 *Au “mafundisho yatatoka.” 2:4 *Au “kurekebisha.”

SURA YA 2

a Isa 1:1

b Zek 8:3

c Zb 72:1, 8
Zb 86:9
Mik 4:1-3
Hag 2:7
Mdo 10:34, 35

d Zek 8:23

e Isa 54:13

f Isa 51:4

Safu ya 2

a Zb 46:9

b Zb 72:7
Isa 60:18
Mt 26:52

c Isa 60:19, 20

d Kum 31:16, 17

e Kum 18:10

f Kum 17:15, 16

g 2Nya 28:1, 2
2Nya 33:1, 7

h Kut 20:18

- Na mikuki yao iwe miundu.^a
- Taifa halitainua upanga dhidi ya taifa lingine, Wala hawatajifunza vita tena kamwe.^b
- 5** Enyi nyumba ya Yakobo, njooni, Na tutembe katika nuru ya Yehova.^c
- 6** Kwa maana umewaacha watu wako, nyumba ya Yakobo,^d Kwa sababu wamejaa vitu vya kutoka Mashariki; Wanafanya uchawi^e kama Wafilisti, Nao wana watoto wengi wa wageni.
- 7** Nchi yao imejaa fedha na dhahabu, Na hazina zao hazina kikomo. Nchi yao imejaa farasi, Na magari yao hayana idadi.^f
- 8** Nchi yao imejaa miungu ya ubatili.^g Wao huinamia kazi ya mikonu yao wenyewe, Kile ambacho vidole vyao vimetengeneza.
- 9** Basi mtu huinama chini, hujishusha chini, Nawe huwezi kuwasamehe.
- 10** Ingia ndani ya mwamba, ujifiche mavumbini Kwa sababu ya uwepo wa Yehova unaogopesha Na fahari yake kuu.^h
- 11** Macho ya mwanadamu yenye majivuno yatashushwa, Na kiburi cha wanadamu kitanama chini.*

2:11 *Au “kitanyenyekezwa.”

Yehova peke yake ndiye atakayekwezwa siku hiyo.

12 Kwa maana hiyo ni siku ya Yehova wa majeshi.^a

Itakuja dhidi ya kila mtu mwenye majivuno na anayejinua,

Itakuja dhidi ya kila mtu, aliyekwezwa au aliye chini,^b

13 Dhidi ya mierezi yote ya Lebanoni ambayo ni miferefu na iliyo juu

Na dhidi ya mialoni yote ya Bashani,

14 Dhidi ya milima yote miferefu

Na dhidi ya vilima vyote virefu,

15 Dhidi ya kila mnara mrefu na kila ukuta wenye ngome,

16 Dhidi ya meli zote za Tarshishi^c

Na dhidi ya mashua zote zinazotamanika.

17 Majivuno ya mwanadamu yatashushwa,

Na kiburi cha wanadamu kitainama chini.*

Yehova peke yake ndiye atakayekwezwa siku hiyo.

18 Miungu ya ubatili itatoweka kabisa.^d

19 Na watu wataingia ndani ya mapango ya miamba Na ndani ya mashimo ardhini,^e

Kwa sababu ya uwepo wa Yehova unaoogopesha Na fahari yake kuu,^f Anapoinuka ili kuifanya dunia itetemeke kwa hofu.

SURA YA 2

a Sef 1:4, 7

b Isa 66:16

c 1Fa 10:22
Eze 27:25

d Isa 27:9

e Ufu 6:15

f Isa 2:10
2Th 1:9

Safu ya 2

a Isa 30:22
Isa 31:7

SURA YA 3

b Law 26:26
Kum 28:49, 51
Yer 37:21
Eze 4:16

c Eze 13:9

d Kut 18:21

e Kum 18:10, 12
Isa 8:19

20 Siku hiyo wanadamu watachukua miungu yao ya ubatili ya fedha na dhababu

Ambayo walijitengenezea ili waiinamie

Na o watawatupia panya* na popo,^a

21 Ili kuingia katika mashimo yaliyo kwenye miamba Na ndani ya mipasuko ya majabali,

Kwa sababu ya uwepo wa Yehova unaoogopesha

Na fahari yake kuu, Anapoinuka ili kuifanya dunia itetemeke kwa hofu.

22 Kwa faida yenu wenyewe, acheni kumtumaini mwanadamu,

Ambaye ni pumzi tu iliyo katika mianzi ya pua yake.*

Kwa nini afikiriwe?

3 Kwa maana tazama! Bwana na kweli, Yehova wa majeshi,

Anaondoa Yerusalemu na Yuda kila aina ya tegemeo na msaada,

Tegemeo lote la kupata mkate na maji,^b

2 Mwanamume hodari na shujaa, Mwamuzi na nabii,^c mbashiri* na mzee,

3 Mkuu wa 50,^d mwanamume mwenye kuheshimiwa, na mshauri,

Mchawi hodari na mlozi stadi.^e

2:20 *Au "wanyama wadogo wanaoguguna ambao hula sana." 2:22 *Au "Ambaye pumzi yake iko katika mianzi ya pua yake." 3:2 *Au "mwaguzi."

2:17 *Au "kitanyenyekezwa."

- 4** Nitawafanya wavulana kuwa wakuu wao, Na watu wanaoyumbayumba* watawatawala.
- 5** Watu watakandamizana, Kila mmoja atamkandamiza mwenzake.^a Mvulana atamshambulia mwanamume mzee, Na mtu asiyeheshimiwa sana atamdharau yule anayeheshimiwa.^b
- 6** Kila mmoja atamshika ndugu yake katika nyumba ya baba yake, na kusema: “Wewe una joho—uwe kamanda wetu. Lisimamie rundo hili la magofu.”
- 7** Lakini siku hiyo atakataa akisema: “Mimi sitakuwa mfungamajeraha* wenu; Sina chakula wala nguo katika nyumba yangu. Msiniweke kuwa kamanda juu ya watu.”
- 8** Kwa maana watu wa Yerusalemu wamejikwaa, Na watu wa Yuda wamea nguka, Kwa sababu wanampinga Yehova kwa maneno na matendo; Wanatenda kwa ukaidi mbele za uwepo wake mtukufu.*^c
- 9** Hali ya nyuso zao inatoa ushahidi dhidi yao, Nazo zinatangaza dhambi yao kama Sodoma;^d Hawajaribu kuificha. Ole wao,* kwa maana wanajiletea msiba!

3:4 *Au “wasio na msimamo.” 3:7 *Au “tabibu.” 3:8 *Tnn., “machoni pa utukufu wake.” 3:9 *Au “Ole wa nafsi zao.”

SURA YA 3

a Yer 9:4, 5
Mik 3:2, 3

b Law 19:32

c 2Nya 33:1, 6
Eze 9:9

d Mwa 18:20
Isa 1:10
Yud 7

Safu ya 2

a Mhu 8:12
Sef 2:3

b Yer 5:31
Hab 1:4

c Isa 1:23
Yer 5:26-28
Mik 2:1, 2
Mik 6:10

d Mik 3:2, 3

- 10** Waambie waadilifu kwamba mambo yatawaendea vema; Watathawabishwa kwa yale wanayotenda.*^a
- 11** Ole wake mtu mwovu! Atapatwa na msiba, Atatendewa yale ambayo mikono yake imetenda!
- 12** Na kuhusu watu wangu, wasimamizi wao wa kazi wanawatesa, Na wanawake huwatawala. Watu wangu, viongozi wenu wanawafanya mtangetange, Nao wanavuruga mwelekeo wa njia zenu.^b
- 13** Yehova anachukua nafasi yake ili kutoa mashtaka; Anasimama ili kuwahukumu watu.
- 14** Yehova atawahukumu wazee na wakuu wa watu wake. “Mmeliteketeza kabisa shamba la mizabibu, Na vitu mlivyowaibia maskini vimo ndani ya nyumba zenu.^c
- 15** Mnawezaje kuwaponda watu wangu Na kusaga nyuso za maskini mavumbini?”^d asema Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi.
- 16** Yehova anasema: “Kwa sababu mabinti wa Sayuni ni wenye majivuno, Nao wanatembea wakiwa wameinua vichwa vyao juu,* Wakipepesa-pepesa macho kwa utongozi,

3:10 *Tnn., “Watakula matunda ya matendo yao.” 3:16 *Tnn., “wakiwa wamerepusha shingo (koo) zao.”

- wakitembea kwa hatua fupifupi,
Wakiwa na vikuku vina-
vyotoa milio kwenye
vifundo vya miguu,
17 Yehova pia atawapiga ma-
binti wa Sayuni kwa
upele kichwani,
Na Yehova atafunua wazi
paji la uso wao.^a
18 Siku hiyo Yehova atao-
ndoa umaridadi wa
bangili zao,
Tepe za kichwani na ma-
pambo yenye umbo la
mwezi mwandamo,^b
19 Herini,* vikuku, na shela,
20 Vitambaa vya kichwani,
mafurungu, na mavazi
ya kifuani,*
Chupa za marashi^c na
hirizi,^d
21 Pete za vidole na pete za
puani,
22 Kanzu za sherehe, kanzu
fupi za nje, majoho, na
mikoba,
23 Vioo vya mkononi^c na
mavazi ya kitani,*
Vilemba na shela.
24 "Badala ya mafuta ya
zeri,^d kutakuwa na
harufu ya uozo;
Badala ya mshipi, kamba;
Badala ya mtindo maridadi
wa nywele, upara;^e
Badala ya vazi lenye tha-
mani, nguo ya magunia;^f
Na alama iliyotiwa mwilini
badala ya urembo.
25 Wanaume wako watauawa
kwa upanga,
Na wanaume wako hodari
watauawa vitani.^g

3:19 *Au "Kigwe." **3:20** *Au "uku-
mbuu." *Tnn., "nyumba za nafsi."
^aAu "kauri zinazovuma zinazotumiwa
kama mapambo." **3:23** *Au "nguo za
ndani."

SURA YA 3

a Isa 3:24

b Amu 8:26

c Kut 38:8

d Est 2:12

e Mik 1:16

f Omb 2:10

g Omb 2:21

Safu ya 2

a Omb 1:4

b Omb 2:10

SURA YA 4

c Isa 3:25

d Mwa 30:22, 23
Lu 1:24, 25e Isa 30:23
Yoe 3:18
Zek 9:17

f Kut 32:32, 33

g Eze 36:25

h Eze 22:20-22

i Kut 13:21
Hes 9:15
Zek 2:4, 5

j Zb 121:5

k Isa 25:4

26 Milango yake italia na kuo-
mboleza,^a

Naye ataketi ardhini kati-
ka hali ya ukiwa."^b

4 Siku hiyo, wanawake saba
watamkamata mwanamu-
me mmoja,^c wakisema:

"Tutakula mkate wetu we-
nyewe

Na kuvaa nguo zetu we-
nyewe;

Lakini turuhusu tu tuitwe
kwa jina lako

Ili kuondoa aibu yetu."^{*d}

2 Siku hiyo kile ambacho
Yehova atachipusha kitakuwa
kizuri sana na chenye utuku-
fu, na mazao ya nchi yataku-
wa kitu cha kujivunia na ure-
mbo kwa ajili ya waokokaji wa
Israeli.^e **3** Yeyote atakayeba-
ki Sayuni na kuachwa Yerusa-
lemu ataitwa mtakatifu, wale
wote walio Yerusalemu walio-
andikwa kwa ajili ya uzima.^f

4 Yehova atakapoosha ucha-
fu wa* mabinti wa Sayuni^g na
kusafisha umwagaji wa damu
wa Yerusalemu kutoka nda-
ni yake kwa roho ya hukumu
na kwa roho ya kuteketeza,^{#h}

5 Yehova pia ataumba juu ya
eneo lote la Mlima Sayuni na
juu ya mahali pa makusanyiko
yake wingu na moshi wakati
wa mchana na moto mwanga-
vu unaowaka wakati wa usi-
ku;ⁱ kwa maana juu ya utu-
kufu wote kutakuwa na maha-
li pa kujificha. **6** Na kutaku-
wa na kibanda chenye kivuli
cha kujikinga na joto wakati
wa mchana,^j nacho kitakuwa
kimbilio na ulinzi wakati wa
dhoruba na mvua.^k

4:1 *Yaani, aibu ya kutoolewa na ku-
tokuwa na watoto. **4:4** *Tnn., "kinyesi
cha." *Au "kuondoa."

- 5** Tafadhali, acha nimwimbie mpenzi wangu Wimbo kuhusu mpenzi wangu na shamba lake la mizabibu.^a
Mpenzi wangu alikuwa na shamba la mizabibu kwenye kilima kinachozaa sana.
- 2** Akalilima na kuondoa mawe ndani yake.
Akapanda mzabibu bora mwekundu,
Akajenga mnara katikati yake,
Naye akachimba shinikizo la divai ndani yake.^b
Kisha akaendelea kutumaini kwamba litazaa zabibu,
Lakini lilizaa zabibu za mwituni peke yake.^c
- 3** “Na sasa, enyi wakaaji wa Yerusalemu na watu wa Yuda,
Tafadhali hukumuni kati yangu na shamba langu la mizabibu.^d
- 4** Ningelifanyia nini kingine shamba langu la mizabibu
Ambacho bado sijafanya?^e
Kwa nini, nilipotumaini kwamba litazaa zabibu,
Lilizaa zabibu za mwituni peke yake?
- 5** Sasa, tafadhali, acheni niwaambie
Kile nitakacholifanyia shamba langu la mizabibu:
Nitaondoa uzio wake,
Nalo litateketezwa kabisa.^f
Nitaubomoa ukuta wake wa mawe,
Nalo litakanyagwa-kanyagwa.
- 6** Nami nitalifanya liwe ukiwa;^g

SURA YA 5

a Zb 80:8
Isa 5:7
Yer 2:21
Lu 20:9

b Mt 21:33
Mk 12:1

c Ho 10:1

d Mik 6:2

e 2Nya 36:15
Eze 24:13

f Law 26:31, 33
Ne 2:3
Zb 79:1

g Kum 29:22, 23
Yer 25:11
Yer 45:4

Safu ya 2

a Isa 32:13

b Kum 11:16, 17

c Zb 80:8
Yer 12:10

d Mik 6:8

e Kum 15:9

f Mik 2:1, 2

g 1Fa 21:15, 16

h 2Nya 36:20, 21
Isa 27:10

i Kum 28:15, 17
Yoe 1:17

Halitapunguzwa matawi wala kulimwa.
Litamea vichaka vya miiba na magugu,^a

Nami nitayaamuru mawingu yasinyeshe mvua yoyote juu yake.^b

7 Kwa maana shamba la mizabibu la Yehova wa majeshi ni nyumba ya Israeli;^c

Watu wa Yuda ndilo shamba alilolipenda sana.
Aliendelea kutumaini haki itendwe,^d

Lakini tazama! kulikuwa na ukosefu wa haki;
Alitumaini uadilifu ufa-nywe,

Lakini tazama! kulikuwa na kilio cha huzuni.”^e

8 Ole wao wanaounganisha nyumba moja na nyingine^f

Na wanaounganisha shamba moja na lingine^g

Mpaka nafasi inapokosekana kabisa

Nanyi mnaishi peke yenu nchini!

9 Yehova wa majeshi ameapa masikioni mwangu

Kwamba nyumba nyingi, ingawa ni kubwa na maridadi,

Zitakuwa kitu cha kutisha, Bila mkaaji.^h

10 Kwa maana ekari kumi za* shamba la mizabibu zitazaa kipimo kimoja tu cha bathi,[#]

Na kipimo kimoja cha homeri[#] ya mbegu kitazaa efa[#] moja tu.ⁱ

5:10 *Tnn., “viganja kumi vya” #Angalia Nyongeza B14.

- 11** Ole wao wanaoamka asu-
buhi na mapema ili
wanywe kileo,^a
Wanaokawia hadi giza li-
napoingia jioni mpaka
divai inapowawasha!
- 12** Wana kinubi na kinanda,
Tari, filimbi, na divai
katika karamu zao;
Lakini hawafikirii utendaji
wa Yehova,
Wala hawaioni kazi ya mi-
kono yake.
- 13** Kwa hiyo watu wangu wa-
taenda uhamishoni
Kwa sababu ya kukosa
ujuzi;^b
Wanaume wao wenye utu-
kufu watakuwa na njaa,^c
Na watu wao wote wata-
kauka kwa kiu.
- 14** Kwa hiyo Kaburi* limeji-
panua[#]
Nalo limefungua kinywa
chake bila kikomo;^d
Na fahari yake,[^] umati
wake wenye kelele, na
watu wake wanaoshere-
hekea
Hakika watashuka na kui-
ngia ndani yake.
- 15** Na mwanadamu atainama,
Mwanadamu atashushwa,
Na macho ya wenye maji-
vuno yatashushwa.
- 16** Yehova wa majeshi ata-
kwezwa kupitia hukumu
yake;^{*}
Mungu wa kweli, Aliye
Mtakatifu,^e atajitakasa
mwenyewe kupitia uadi-
lifu.^f
- 17** Na wanakondoo watalisha
kama katika malisho yao;

5:14 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uk. 2012. [#]Au "limepanua nafsi yake."
[^]Au "wakuu wake." 5:16 *Au "haki yake."

SURA YA 5

a Lu 21:34
Ro 13:13

b Isa 27:11
Yer 8:7
Ho 4:6

c Omb 4:9

d Kum 28:63

e Isa 6:3
Ufu 4:8

f Kum 32:4

Safu ya 2

a Yer 5:12
Yer 17:15
Eze 12:22

b Met 17:15
Mal 2:17

c Met 3:7
Ro 12:16

d Met 23:20
Met 31:4, 5

e Kum 16:19
Isa 1:23
Mik 3:11

f 1Fa 21:13
Met 17:15

Wakaaji wageni watakula
katika maeneo yenye
ukiwa ya wanyama walio-
lishwa vizuri.

- 18** Ole wao wanaokokota ha-
tia yao kwa kamba za
udanganyifu
Na dhambi yao kwa kamba
za gari la kukokotwa;
- 19** Wale wanaosema: "Na
aharakishe kazi yake;
Na ije upesi ili tuione.
Kusudi la* Mtakatifu wa
Israeli na litimizwe
Ili tulijue!"^a
- 20** Ole wao wanaosema kwa-
mba wema ni uovu na
uovu ni wema,^b
Wale wanaoweka giza ba-
dala ya nuru na nuru
badala ya giza,
Wale wanaoweka uchungu
badala ya utamu na uta-
mu badala ya uchungu!
- 21** Ole wao walio na
hekima katika macho
yao wenyewe
Na walio na busara macho-
ni pao wenyewe!^c
- 22** Ole wao walio hodari kati-
ka kunywa divai
Na wanaume walio
stadi katika kuchanga-
nya vileo,^d
- 23** Wale wanaomwondolea
mwovu hatia kwa ru-
shwa^e
Na wanaomnyima haki
mwadilifu!^f
- 24** Kwa hiyo, kama mwali
wa moto unavyoteketeza
majani makavu
Na majani makavu yana-
vyonyauka katika moto,
Mizizi yao wenyewe itaoza,
Na maua yao yatatawanyika
kama ungaunga,

5:19 *Au "Uamuzi wa; Shauri la."

Kwa sababu walikataa she-
ria* ya Yehova wa
majeshi,
Na kulidharau neno la
Mtakatifu wa Israeli.^a

25 Ndiyo sababu hasira ya
Yehova inawaka dhidi
ya watu wake,
Naye ataunyoosha mkono
wake dhidi yao na kuwa-
piga.^b

Milima itatetemeka,
Na maiti zao zitakuwa
kama takataka bara-
barani.^c

Kwa sababu ya hayo yote,
hasira yake haijapoa,
Lakini mkono wake bado
umenyoosha ili kupiga.

26 Ameliinulia ishara* taifa
lililo mbali;^d
Amewapigia mluzi waje
kutoka miishi ya dunia;^e
Na tazama! wanakuja
upesani sana.^f

27 Hakuna yeyote kati yao
aliyechoka wala kuji-
kwaa.

Hakuna yeyote anayesi-
nzia au kulala.

Mshipi ulio kwenye kiuno
chao haujalegezwa,
Wala kamba za viatu vyao
hazijakatika.

28 Mishale yao yote ni mikali,
Na pinde zao zote zimepi-
ndika.*

Kwato za farasi wao ni
kama jiwe gumu lenye
makali,
Na magurudumu yao kama
upepo wa dhoruba.^g

29 Mngurumo wao ni kama
wa simba;

5:24 *Au "mafundisho." 5:26 *Au
"nguzo ya ishara." 5:28 *Au "ziko
tayari kupiga mshale."

SURA YA 5

a Kum 31:20
2Fa 17:13, 14
Ne 9:26
Isa 1:4

b Kum 31:16, 17
2Nya 36:15, 16
Omb 2:2

c Yer 16:4

d Yer 52:4

e Kum 28:49, 50
Yer 5:15

f Yer 4:13

g Hab 1:8

Safu ya 2

a Yer 50:17

b Yer 6:23

c Yer 4:23

SURA YA 6

d 2Nya 26:23

e 1Fa 22:19
Da 7:9

f Kut 15:11
Ufu 4:8

g Ufu 15:8

Wananguruma kama wa-
nasimba.*^a

Watanguruma na kukama-
ta mawindo

Na kuyabeba bila mtu wa
kuyaokoa.

30 Siku hiyo watanguruma
juu yake
Kama mngurumo wa
bahari.^b

Mtu yeyote anayeitazama
nchi ataona giza lenye
kutaabisha;

Hata nuru imetiwa giza
kwa sababu ya
mawingu.^c

6 Katika mwaka ambao Mfal-
me Uzia alikufa,^d nilimwo-
na Yehova akiwa ameketi kwe-
nye kiti cha ufalme kilicho juu
na kilichoinuliwa,^e na pindo
za kanzu yake zilijaa hekalu-
ni. **2** Maserafi walikuwa wa-
mesimama juu yake; kila
mmoja wao alikuwa na maba-
wa sita. Kila mmoja alifunika
uso wake kwa mabawa ma-
wili na alifunika miguu yake
kwa mawili, na kila mmoja
wao aliruka huku na huku kwa
mawili.

3 Na kila mmoja alimwa-
mbia mwenzake:

"Mtakatifu, mtakatifu,
mtakatifu ni Yehova wa
majeshi.^f

Dunia yote imejaa utukufu
wake."

4 Na viegemeo vya milango
vikatetemeka kwa sababu ya
ile sauti kubwa,* na nyumba
ikajaa moshi.^g

5 Kisha nikasema: "Ole
wangu!

5:29 *Au "wanasimba wenye manyoya
marefu shingoni." 6:4 *Tnn., "sauti ya
yule aliyekuwa akiita."

Kwa maana ni kama nimekufa,*

Kwa maana mimi ni mtu asiye na midomo safi, Nami ninaishi kati ya watu wasio na midomo safi;^a

Kwa maana macho yangu yamemwona Mfalme, Yehova wa majeshi mwenyewe!”

6 Ndipo mmoja wa maserafi akaruka kunijia, na mkono ni mwake alikuwa na kaa linalowaka^b alilokuwa amechukua kwa koleo kutoka kwenye madhabahu.^c **7** Akakigusa kinywa changu na kusema:

“Tazama! Hili limeigusa midomo yako.

Hatia yako imeondolewa, Na dhambi yako imefunikwa.”

8 Kisha nikasikia sauti ya Yehova ikiuliza: “Nimtume nani, na ni nani atakayenda kwa ajili yetu?”^d Nami nikasema: “Mimi hapa! Nitume mimi!”^e

9 Ndipo akasema, “Nenda, uwaambie hivi watu hawa:
‘Mtasikia tena na tena, Lakini hamtaelewa;
Mtaona tena na tena, Lakini hamtapata ujuzi wowote.’^f

10 Ufanye moyo wa watu hawa uwe mgumu,^g Yafanye masikio yao yawe mazito,^h
Na uyafunge kabisa macho yao,
Ili wasione kwa macho yao
Na wasisikie kwa masikio yao,
Ili moyo wao usielewe

6:5 * Tnn., “nimenyamazishwa.”

SURA YA 6

a Isa 29:13

b Eze 10:2

c Ufu 8:5

d Mwa 1:26
Yoh 1:1, 2
Yoh 12:41

e Zb 110:3
Mt 4:19, 20

f Yer 5:21
Mt 13:14
Lu 8:9, 10
Mdo 28:25, 26

g Eze 3:7

h Yer 6:10
Yoh 3:20

Safu ya 2

a Mt 13:15
Mdo 28:27

b 2Nya 36:20, 21
Isa 3:26
Isa 24:1

c 2Fa 25:11

SURA YA 7

d 2Fa 16:1, 2

e 2Fa 15:37
2Nya 28:6

f 2Fa 16:5

g Isa 8:18

h 2Fa 18:17

Nao wasigeuke na kuponywa.”^a

11 Ndipo nikauliza: “Ni mpaka lini, Ee Yehova?” Kisha akasema:

“Mpaka majiji yabomoke yawe magofu bila mkaaji Na nyumba zisiwe na watu Na nchi iharibiwe na kuba-ki ukiwa;^b

12 Mpaka Yehova awaondoe watu na kuwapeleka mbali^c
Na hali ya ukiwa ya nchi ienee sana.

13 “Lakini bado kutakuwa na sehemu ya kumi ndani yake, nayo itateketezwa tena, kama mti mkubwa na kama mwaloni, ambayo inapokatwa huacha kisiki; mbegu takatifu itakuwa* kisiki chake.”

7 Sasa katika siku za Ahazi^d mwana wa Yothamu mwana wa Uzia, mfalme wa Yuda, Mfalme Resini wa Siria na Peka^e mwana wa Remalia, mfalme wa Israeli, walipanda ili kuja kupigana vita dhidi ya Yerusalemu, lakini alishindwa* kuliteka.^f **2** Habari ikapelekwa kwa nyumba ya Daudi: “Siria imeungana na Efraimu.”

Na moyo wa Ahazi na moyo wa watu wake ukaanza kute-temeka, kama miti ya msituni inavyotikiswa na upepo.

3 Kisha Yehova akamwambia Isaya: “Tafadhali ondo-ka, wewe na mwana wako Shear-yashubu,^g uende kuku-tana na Ahazi, kwenye mwisho wa mfereji^h wa kidimbwi cha juu^h karibu na barabara

6:13 *Au “uzao mtakatifu utakuwa.”
7:1 *Au labda, “walishindwa.” **7:3** *Maana yake “Ni Mabaki tu Watakaorudi.” *Au “mtaro wa maji.”

kuu ya uwanja wa mfuaji wa nguo. **4** Umwambie, 'Jitahidi kuwa mtulivu. Usiogope, na usivunjike moyo kwa sababu ya haya magogo mawili yanayotoa moshi, kwa sababu ya hasira kali ya Resini na Siria na mwana wa Remalia.^a **5** Kwa maana Siria pamoja na Efraimu na mwana wa Remalia wamepanga njama ya kukuhuru, wakisema: **6** "Na tupande dhidi ya Yuda na kuirarua* na kuishinda[#] iwe yetu, nasi tumweke mwana wa Ta-beeli kuwa mfalme wake."^b

7 "“Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Haitafanikiwa,
Wala haitatimia.

8 Kwa maana kichwa cha Siria ni Damasko,

Na kichwa cha Damasko ni Resini.

Katika muda wa miaka 65 tu

Efraimu litavunjwa kabisa na halitakuwa taifa tena.^c

9 Kichwa cha Efraimu ni Samaria,^d

Na kichwa cha Samaria ni mwana wa Remalia.^e

Msipokuwa na imani thabiti,
Hamtakuwa imara.””

10 Yehova akaendelea kumwambia Azazi: **11** “Mwombe Yehova Mungu wako^f ishara; inaweza kuwa yenye kina kama Kaburi* au iwe juu kama anga.” **12** Lakini Azazi akasema: “Sitaomba, wala sitamjaribu Yehova.”

7:6 *Au labda, “kuishambulia.” [#]Au “bomoa kuta zake.” Tnn., “kulipasua.” 7:11 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 7

a 2Fa 15:30
Isa 8:6, 7

b 2Fa 16:5

c 2Fa 17:6
Ho 1:6

d 1Fa 16:23, 24

e 2Fa 15:27

f Amu 6:36, 37
Isa 37:30
Isa 38:7, 8

Safu ya 2

a 2Nya 36:15, 16

b Isa 9:6
Yoh 1:14
1Ti 3:16

c Mt 1:23
Lu 1:30-35

d 2Fa 15:29
2Fa 16:8, 9
Isa 8:3, 4
Isa 17:1

e 1Fa 12:20

f 2Fa 18:13, 14
2Nya 28:19, 20
Isa 36:1

g 2Fa 16:7

13 Kisha Isaya akasema: “Tafadhali, sikilizeni, enyi nyumba ya Daudi. Je, haitoshi kwamba mnaijaribu subira ya wanadamu? Je, ni lazima pia mujaribu subira ya Mungu?^a **14** Kwa hiyo Yehova mwenyewe atawapa ishara: Tazama! Mwanamke kijana* atapata mimba naye atazaa mwana,^b na kumwita jina Imanueli.^{#c} **15** Atakula siagi na asali kufikia wakati atakapojua jinsi ya kukataa lililo baya na kuchagua lililo jema. **16** Kwa maana kabla ya mvulana huyo kujua jinsi ya kukataa lililo baya na kuchagua lililo jema, nchi ya wale wafalme wawili mnaowahofu itaachwa kabisa.^d **17** Yehova ataleta dhidi yako na dhidi ya watu wako na dhidi ya nyumba ya baba yako wakati ambao haujawahi kuonekana tangu Efraimu lilipojitenga na Yuda,^e kwa maana Yeye atamleta mfalme wa Ashuru.^f

18 “Siku hiyo Yehova atawapigia mluzi nzi kutoka katika vijito vya mbali vya Mto Nile wa Misri na nyuki kutoka katika nchi ya Ashuru, **19** nao wote watakuja na kutua kwenye mabonde yenye mteremko mkali,* kwenye mipasuko ya miamba, kwenye vi-chaka vyote vya miiba, na sehemu zote za kunyweshea.

20 “Siku hiyo, kwa kutumia wembe uliokodiwa kutoka eneo la ule Mto,* kwa kumtumia mfalme wa Ashuru,^g Yehova atanyoa kichwa na nywele za miguu, nao utafagilia mbali ndevu pia.

7:14 *Au “Mwanamwali.” [#]Maana yake “Mungu Yuko Pamoja Nasi.” 7:19 *Au “makorongo.” 7:20 *Yaani, Mto Efrati.

21 “Siku hiyo mtu atamhifadhi hai ng’ombe mchanga aliye kundini na kondoo wawili. 22 Na kwa sababu ya wingi wa maziwa, atakula siagi, kwa maana kila mtu anayebaki katika nchi atakula siagi na asali.

23 “Siku hiyo mahali popote palipokuwa na mizabibu 1,000 yenye thamani ya vipande 1,000 vya fedha, patakuwa na vichaka vya miiba na magugu peke yake. 24 Watu wataenda huko wakiwa na mishale na upinde, kwa sababu nchi yote itakuwa vichaka vya miiba na magugu. 25 Na milima yote iliyokuwa ikilimwa kwa jembe, hutaikaribia kwa kuogopa vichaka vya miiba na magugu; itakuwa mahali pa kulisha ng’ombe na mahali pa kukanyagwa na kondoo.”

8 Yehova akaniambia: “Chukua bamba kubwa^a na uandike juu yake kwa kalamu ya kawaida,* ‘Maher-shalal-hash-bazi.’” 2 Nami nihakikishe kwamba limethibitishwa kwa maandishi* na mashahidi waaminifu, kuhani Uriah^b na Zekaria mwana wa Yeberekia.”

3 Ndipo nikalala na* yule nabii wa kike,[#] naye akapata mimba na baada ya muda akazaa mwana.^c Kisha Yehova akaniambia: “Mwite jina Maher-shalal-hash-bazi, 4 kwa maana kabla mvulana huyo hajajua jinsi ya kuita, ‘Baba yangu!’ na ‘Mama yangu!’ mali za Damasko na

8:1 *Tnn., “kalamu ya mwanadamu anayeweza kufa.” #Huenda jina hili linamaanisha “Kuharakisha Kwenda Kwenye Nyara, Kuja Upesi Kwenye Nyara.” 8:2 *Au “limeshuhudiwa.” 8:3 *Tnn., “nikamkaribia.” #Yaani, mke wa Isaya.

SURA YA 8

a Isa 30:8

b 2Fa 16:10

c Isa 8:18

Safu ya 2

a 2Fa 15:29

2Fa 16:8, 9

2Fa 17:6

Isa 7:16

Isa 17:1

b 2Fa 17:16

Yer 17:13

c Isa 7:1

d 2Fa 17:5

2Fa 18:9

e 2Nya 28:19, 20

Isa 7:17, 20

Isa 10:28-32

f Isa 7:14

Mt 1:23

g 2Nya 32:21

nyara za Samaria zitachukuliwa mbele ya mfalme wa Ashuru.”^a

5 Yehova akaniambia tena:

6 “Kwa sababu watu hawa wamekataa maji ya Shiloa* yanayotiririka polepole^b

Nao wanamshangilia Resini na mwana wa Remalia,^c

7 Kwa hiyo tazama! Yehova ataleta dhidi yao Maji yenye nguvu na yaliyo mengi ya ule Mto,* Mfalme wa Ashuru^d na utukufu wake wote.

Atakuja juu ya sakafu zake zote za vijito Na kufurika kwenye kingo zake zote

8 Na kupita katika nchi yote ya Yuda.

Atafulika na kuvuka, na kufika shingoni;^e

Mabawa yake yaliyonyoosha yatajaza upana wa nchi yako,

Ewe Imanueli!”^{*f}

9 Sababisheni madhara, enyi watu, lakini mtavunjwa vipandevipande.

Sikilizeni, nyote mnaotoka sehemu za mbali za dunia!

Jitayarisheni kwa ajili ya vita,* lakini mtavunjwa vipandevipande!^g

Jitayarisheni kwa ajili ya vita, lakini mtavunjwa vipandevipande!

10 Fanyeni mpango, lakini utavunjwa!

Semeni mnachotaka, lakini hakitafanikiwa,

8:6 *Shiloa ulikuwa mfereji wa maji.

8:7 *Yaani, Mto Efrati. 8:8 *Angalia

Isa 7:14. 8:9 *Au “Jifungeni viuno.”

Kwa maana Mungu yuko pamoja nasi! *^a

11 Kwa mkono wake wenye nguvu ulio juu yangu, Yehova aliniambia hivi ili kunionya nisifuuate njia ya watu hawa:

12 “Usikiite njama kitu ambacho watu hawa wanakiita njama! Usiogope kitu wanachoo-gopa;

Usitetemeshwe nacho.

13 Yehova wa majeshi—Yeye ndiye mnayepaswa kumwona kuwa mtakatifu,^b Yeye ndiye mnayepaswa kumwogopa, Na Yeye ndiye anayepaswa kuwatetemesha ninyi.”^c

14 Atakuwa kama mahali patakatifu, Lakini kama jiwe la kujinganga juu yake Na kama mwamba wa kujikwaa juu yake^d Kwa nyumba zote mbili za Israeli, Kama mtego na kama kitu kinachonasa Kwa wakaaji wa Yerusalemu.

15 Wengi wao watajikwaa na kuanguka na kuvunjwa; Watanaswa na kuka-matwa.

16 Funga ule uthibitisho ulioandikwa,^{*} Tia muhuri sheria[#] kati ya wanafunzi wangu!

17 Nitaendelea kumtarajia * Yehova,^e ambaye anauficha uso wake kutoka kwa nyumba

8:10 *Katika Kiebrania maana ya neno *Imanueli* ni “Mungu yuko pamoja nasi.” Angalia Isa 7:14; 8:8. **8:16, 20** *Au “ushahidi.” **8:16** #Au “mafundisho.” **8:17** *Au “kumsubiri kwa hamu.”

SURA YA 8

a Kum 20:1
Zb 44:3

b Law 10:3
Law 22:32

c Mhu 12:13
Mt 10:28

d Mt 21:42, 44
Lu 20:17, 18
Ro 9:31-33
1Ko 1:23
1Pe 2:7, 8

e Zb 33:20

Safu ya 2

a Kum 31:16, 17
Mik 3:4

b Ebr 2:13

c Isa 7:14, 16
Isa 8:3, 4

d Law 20:6
Kum 18:10, 11
Zb 146:4
Mhu 9:5, 10

e Met 4:19

f Kum 28:15, 48

SURA YA 9

g 2Fa 15:29

ya Yakobo,^a nami nitamtu-mainia.

18 Tazama! Mimi na wato-to ambao Yehova amenipa^b ni kama ishara^c na kama miuji-za katika Israeli kutoka kwa Yehova wa majeshi, anayekaa kwenye Mlima Sayuni.

19 Nao wakiwaambia: “Tafuteni habari kutoka kwa wale wanaowasiliana na roho au wabashiri wanaonong’oneza na kutoa sauti za chini,” je, watu hawapaswi kutafuta habari kutoka kwa Mungu wao? Je, wanapaswa kutafuta habari kutoka kwa wafu kwa ajili ya walio hai?^d **20** Badala yake, wanapaswa kutafuta habari katika sheria na uthibitisho ulioandikwa!^{*}

Wasiposema kulingana na neno hili, hawana nuru.^{#e}

21 Na kila mtu atapita katika nchi akiteseka na akiwa na njaa;^f na kwa sababu ana njaa na ghadhabu, atamtukana mfalme wake na Mungu wake huku akitazama juu.

22 Kisha ataiangalia dunia na kuona taabu na giza peke yake, gizagiza na nyakati ngumu, na utusitusi bila mwangaza.

9 Hata hivyo, utusitusi huo hautakuwa kama nchi ilipokuwa na taabu, kama nyakati za zamani nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali zilipodharauliwa.^g Lakini baadaye Yeye ataifanya iheshimiwe—njia iliyo kando ya bahari, katika eneo la Yordani, Galilea ya mataifa.

2 Watu waliokuwa wakite-mbea gizani
Wameona nuru kuu.

8:20 #Tnn., “mapambazuko.”

Na wale wanaokaa katika nchi ya kivuli kizito, Nuru imewaangazia.^a

- 3** Umelifanya taifa hilo liwe na watu wengi;

Umefanya shangwe yake iwe kubwa

Wanashangilia mbele zako
Kama watu wanavyoshangilia wakati wa mavuno,
Kama wale wanaogawana nyara kwa shangwe.

- 4** Kwa maana umeivunjavunja nira ya mzigo wao, Fimbo iliyo kwenye mabega yao, gongo la msimamizi wa kazi, Kama katika siku ya Midiani.^b

- 5** Kila kiatu cha askari kinachotikisa dunia kinapopiga mwendo
Na kila vazi lililoloweshwa katika damu
Litakuwa kuni kwa ajili ya moto.

- 6** Kwa maana mtoto ameza-liwa kwetu,^c
Tumepewa mwana
Na utawala* utakaa juu ya bega lake.^d
Jina lake litakuwa Mshauri wa Ajabu,^e Mungu Mwenye Nguvu,^f Baba wa Milele, Mkuu wa Amani.

- 7** Kwa wingi wa utawala wake*
Na amani, hakutakuwa na mwisho,^g
Kwenye kiti cha ufalme cha Daudi^h na juu ya ufalme wake
Ili kuuimarisha kabisaⁱ na kuutegemeza
Kupitia haki^j na uadilifu,^k

9:6 *Au "serikali; utawala wa kifalme."

9:7 *Au "serikali yake; utawala wake wa kifalme."

SURA YA 9

a Mt 4:13-16
Lu 1:78, 79
Lu 2:30-32
Yoh 1:9
Yoh 8:12

b Amu 8:12, 28
Isa 10:26, 27

c Lu 1:35
Lu 2:11

d Mwa 49:10
Zb 2:6
Zek 6:13
Lu 22:29
Ufu 19:16

e Isa 11:2
Mt 7:28, 29
Mt 12:42

f Zb 45:3
Yoh 1:18

g Zb 72:1, 7
Da 2:44

h Lu 1:32, 33

i 2Sa 7:16, 17
Ufu 11:15

j Isa 42:1
Mt 12:18

k Zb 45:6
Isa 32:1
Yer 23:5
Ebr 1:8

Safu ya 2

a 2Fa 17:6

b Amo 5:11

c 2Nya 28:18

d Kum 31:17

e Isa 5:25
Isa 10:4

f 2Fa 17:13, 14
Ho 7:10
Amo 4:6
Amo 5:6

g 2Fa 17:6
Ho 10:15

Kuanzia sasa mpaka milele.

Bidii ya Yehova wa majeshi itafanya hayo.

- 8** Yehova alituma neno dhidi ya Yakobo, Nalo limekuja dhidi ya Israeli.^a

- 9** Na watu wote watalijua —Efraimu na wakaaji wa Samaria— Ambao wanasema kwa kiburi chao na mioyo yao yenye dharau:

- 10** "Matofali yameanguka, Lakini tutajenga kwa mawe yaliyochongwa.^b Mikuyu imekatwa, Lakini tutaweka mierezi badala yake."

- 11** Yehova atawainua wapi-nzani wa Resini dhidi yake
Naye atawachochea maa-
dui wake wachukue hatua,

- 12** Siria kutoka mashariki na Wafilisti kutoka magharibi,^{*c}
Watamnyafua Israeli kwa vinywa vilivyo wazi.^d
Kwa sababu ya hayo yote, hasira yake haijapoa, Lakini mkono wake bado umenyooshwa ili kupiga.^e

- 13** Kwa maana watu hawajarudi kwa Yule anayewapiga; Hawajamtafuta Yehova wa majeshi.^f

- 14** Yehova atakata kabisa kutoka Israeli
Kichwa na mkia, chipukizi na utete,^{*g} katika siku moja.^g

9:12 *Tnn., "kutoka nyuma." 9:14 *Au labda, "tawi la mtende na tete."

- 15** Mzee na anayeheshimiwa sana ndiye kichwa, Na nabii anayetoa mafundisho ya uwongo ndiye mkia.^a
- 16** Wale wanaowaongoza watu hawa wanawafanya watangetange; Na wale wanaoongozwa wamevurugika.
- 17** Ndiyo sababu Yehova hatawashangilia vijana wao, Naye hatawaonyesha rehema mayatima wao na wajane wao; Kwa sababu wote ni waasi imani na watenda maovu.^b Na kila kinywa kinasema kwa upumbavu. Kwa sababu ya hayo yote, hasira yake haijapoa, Lakini mkono wake bado umenyooshwa ili kupiga.^c
- 18** Kwa maana uovu unawaka kama moto, Ukiteketeza vichaka vya miiba na magugu. Utawasha moto vichaka vya msitu, Navyo vitapanda juu kati-ka mwingu ya moshi.
- 19** Katika ghadhabu ya Yehova wa majeshi Nchi imewashwa moto, Na watu watakuwa kuni kwa ajili ya huo moto. Hakuna yeyote atakayemhurumia hata ndugu yake.
- 20** Mtu atakata upande wa kulia Lakini bado atakuwa na njaa, Na mtu atakula upande wa kushoto

SURA YA 9

a Kum 13:1-3

b Kum 4:25, 26

c Isa 5:25

Safu ya 2

a 2Nya 28:6

b Isa 5:25

SURA YA 10

c Law 19:15
Kum 1:16, 17

d Amo 2:7, 8

e Kum 27:19
Yak 1:27

f Ho 9:7

g Kum 28:49, 50

h Ho 5:13

i Isa 5:25
Isa 9:12

Lakini hatashiba.
Kila mtu atainyafua
nyama ya mkono wake
mwenyewe,

- 21** Manase atamnyafua Efraimu,
Na Efraimu atamnyafua Manase.
Wote pamoja watapigana na Yuda.^a
Kwa sababu ya hayo yote, hasira yake haijapoa, Lakini mkono wake bado umenyooshwa ili kupiga.^b

10 Ole wao wanaotunga sheria zinazodhuru,^{*c}

Ambao sikuzote huandika amri zinazokandamiza,

- 2** Ili kuwanyima maskini haki zao za kisheria, Ili kuwanyang'anya haki watu wa hali ya chini kati ya watu wangu,^d
Kuafanya wajane kuwa nyara yao
Na kuwaporaa mayatima!^e
- 3** Mtafanya nini katika siku ya kuadhibiwa,^{*f}
Uharibifu utakapokuja kutoka mbali?^g
Mtamkimbilia nani ili kupata msaada^h
Nanyi mtauacha wapi utajiri[#] wenu?
- 4** Hakuna kinachobaki isipokuwa kujikunyata kati ya wafungwa
Au kuanguka kati ya waliouawa.
Kwa sababu ya hayo yote, hasira yake haijapoa, Lakini mkono wake bado umenyooshwa ili kupiga.ⁱ

10:1 *Au "masharti yanayodhuru."

10:3 *Au "kuwajibishwa." #Au "utukufu."

- 5** “Aha! Mwashuru,^a
Fimbo ya kuonyesha hasira yangu,^b
Na gongo lililo mkononi mwao kwa ajili ya shutuma yangu!
- 6** Nitamtuma yeye dhidi ya taifa lililoasi imani,^c
Dhidi ya watu walionikasisisha,
Nitamwamuru achukue nyara nyingi na kupora mali nyingi
Na kuzikanyaga kama matope barabarani.^d
- 7** Lakini hatataka kufanya hivyo
Na moyo wake hautapanga hila kwa njia hiyo;
Kwa maana moyo wake umeazimia kuangamiza
Kuangamiza kabisa mataifa mengi, si machache.
- 8** Kwa maana anasema,
‘Je, wakuu wangu wote si wafalme?’^e
- 9** Je, Kalno^f si kama tu Kar-kemishi?^g
Je, Hamathi^h si kama Arpadi?ⁱ
Je, Samaria^j si kama Damasko?^k
- 10** Mkono wangu umeziteka falme za miungu ya ubatili,
Ambazo sanamu zao za kuchongwa zilikuwa nyingi kuliko zile za Yerusalemu na Samaria!^l
- 11** Je, sitaitendea pia Yerusalemu na sanamu zake
Kama vile nilivyoitendea Samaria na miungu yake ya ubatili?’^m
- 12** “Yehova atakapomaliza kazi yake yote kwenye Mlima Sayuni na Yerusalemu, ata-

SURA YA 10

a Mwa 10:9, 11

b 2Fa 17:3
Isa 8:3, 4
Isa 10:24

c 2Fa 17:6

d Kum 28:45, 63
2Fa 17:22, 23

e 2Fa 18:19, 24

f Amo 6:2

g 2Nya 35:20

h 2Fa 17:24

i 2Fa 19:11, 13

j 2Fa 17:5
2Fa 18:9, 10

k 2Fa 16:8, 9

l 2Fa 19:17, 18

m 2Fa 18:33, 34
2Nya 32:16, 19

Safu ya 2

a 2Fa 18:19
2Fa 18:28, 35b 2Fa 15:29
2Fa 17:6
2Fa 18:11
1Nya 5:26c 2Fa 16:8
2Fa 18:16

d 2Fa 18:19, 25

e Isa 10:5

f 2Nya 32:21

g Isa 30:30, 31

h Zb 84:11

i Isa 9:5
Isa 30:27
Isa 31:8, 9
Nah 1:6

mwadhibu* mfalme wa Ashuru kwa sababu ya moyo wake wenye dharau na macho yake yanayotazama kwa kiburi na majivuno.^a **13** Kwa maana anasema,

‘Nitafanya hivyo kwa nguvu za mkono wangu
Na kwa hekima yangu, kwa maana nina hekima.
Nitaiondoa mipaka ya mataifa^b
Na kupora hazina zao,^c
Nami nitawatiisha wakaaji kama mwenye nguvu.^d

14 Kama mtu anayeingiza mkono katika kiota,
Mkono wangu utateka mali za mataifa;
Na kama mtu anayekusanya mayai yaliyoachwa,
Nitaikusanya dunia nzima!
Hakuna atakayepiga mabawa yake au kufungua kinywa chake wala kuno-ng’oneza.’”

15 Je, shoka litajikweza juu ya yule anayelitumia kukata?
Je, msumeno utajikweza juu ya yule anayeutumia kukata?
Je, gongo^e linaweza kumtikisa yule anayeliinua?
Au je, fimbo inaweza kumwinua yule ambaye hajatengenezwa kwa mbao?

16 Kwa hiyo Bwana wa kweli, Yehova wa majeshi,
Atawafanya watu wake walionenepa wakonde,^f
Na chini ya utukufu wake atawasha moto mkubwa unaoteketeza.^g

17 Nuru^h ya Israeli itakuwa moto,ⁱ

10:12 * Tnn., “nitamwadhibu.”

Na Mtakatifu wake mwali wa moto;

Utawaka na kutekeleza magugu yake na vichaka vyake vya miiba kwa siku moja.

18 Ataondoa kabisa* utukufu wa msitu wake na shamba lake la matunda; Itakuwa kama mtu mgonjwa anavyodhoofika.^a

19 Miti itakayobaki katika msitu wake Itakuwa michache sana hivi kwamba mvulana ataweza kuihesabu.

20 Siku hiyo watu wa Israeli waliobaki Na waliookoka wa nyumba ya Yakobo

Hawatamtegemea tena yule aliyewapiga;^b

Bali watamtegemea Yehova,

Mtakatifu wa Israeli, kwa uaminifu.

21 Ni watu wachache tu waliobaki watakaorudi, Watu wa Yakobo waliobaki, watarudi kwa Mungu Mwenye Nguvu.^c

22 Kwa maana ingawa watu wako, ewe Israeli, Ni kama chembe za mchanga wa bahari, Ni watu wachache tu waliobaki watakaorudi.^d Maangamizi yameamuliwa,^e

Na haki* itawafunika.^f

23 Naam, maangamizi yaliyoamuliwa na Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi,

SURA YA 10

a Isa 37:36

b 2Nya 28:20, 21
Ho 5:13
Ho 14:3

c Isa 65:9
Ho 1:10, 11

d Isa 1:9

e Isa 28:22

f Ro 9:27, 28

Safu ya 2

a Kum 28:45, 63

b 2Fa 18:13
Isa 10:5

c Kut 14:3, 9

d 2Fa 19:35

e 2Nya 32:21
Isa 30:32
Nah 3:7

f Amu 7:25
Amu 8:21
Zb 83:11

g Kut 14:21, 27

h Isa 9:4
Nah 1:13

i Isa 14:25

j 2Fa 19:35
Isa 37:35, 36

k Yos 7:2

l Isa 13:2
Isa 14:31

m Yos 21:8, 17
2Nya 16:6

n Amu 20:13

o Ho 5:8

p Yos 21:8, 18
Yer 1:1

q 1Sa 22:18, 19

Yatatekelezwa katika nchi yote.^a

24 Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, anasema: “Msiogope, watu wangu mnaokaa Sayuni, kwa sababu ya Mwashuru, aliyekuwa akiwapiga kwa fimbo^b na kuinua gongo lake dhidi yenu kama Misri ilivyofanya.^c

25 Kwa maana kwa muda mfupi sana shutuma itafika mwisho; hasira yangu itaelekezwa kwenye maangamizi yao.^d **26** Yehova wa majeshi atatikisa mjeledi dhidi yake,^e kama aliposhinda Midiani kando ya mwamba wa Orebu.^f Na gongo lake litakuwa juu ya bahari, naye ataliinua kama alivyoitendea Misri.^g

27 “Siku hiyo mzigo wake utaondoka juu ya bega lako,^h

Na nira yake itaondoka kwenye shingo yako,ⁱ

Na nira itavunjwa/ kwa sababu ya mafuta.”

28 Amekuja Aiathi;^k Amepitia Migroni; Ameweka mizigo yake huko Mikmashi.^l

29 Wamevuka kivuko; Wamekaa Geba usiku kucha;^m

Rama inatetemeka, Gibeaaⁿ ya Sauli imekimbia.^o

30 Paza sauti yako na upige mayowe, Ee binti ya Galimu!

Sikiliza, Ee Laisha!

Ewe maskini Anathothi!^p

31 Madmena amekimbia. Wakaaji wa Gebimu wametafuta mahali pa kujificha.

32 Leo hiihi atasimama Nobu.^q

10:18 *Au “Kuanzia kwenye nafsi hadi kwenye mwili ataondoa.” 10:22 *Au “adhabu.”

Anautikisia ngumi mlima
wa binti ya Sayuni,
Kilima cha Yerusalemu.

33 Tazama! Bwana wa kweli,
Yehova wa majeshi,
Anakata matawi kwa ki-
shindo kikubwa sana;^a
Miti mirefu zaidi inakatwa,
Na walio juu wanashu-
shwa.

34 Anapiga vichaka vya msitu
kwa kifaa cha chuma,^{*}
Na Lebanoni utaangushwa
na mwenye nguvu.

11 Na tawi^b litakua kutoka
kwenye kisiki cha
Yese,^c

Na chipukizi^d kutoka kwe-
nye mizizi yake litazaa
matunda.

2 Na roho ya Yehova itatua
juu yake,^e

Roho ya hekima^f na ya ue-
lewaji,

Roho ya shauri na ya
nguvu,^g

Roho ya ujuzi na ya ku-
mwogopa Yehova.

3 Naye atafurahia kumwo-
gopa Yehova.^h

Hatahukumu kwa mambo
anayoona kwa macho
yake,

Wala kukaripia kulingana
tu na mambo anayosikia
kwa masikio yake.ⁱ

4 Atawahukumu kwa haki^{*}
watu wa hali ya chini,
Na kwa unyofu atakaripia
kwa ajili ya wapole wa
dunia.

Ataipiga dunia kwa fimbo
ya kinywa chake^j

Na kuwaua waovu kwa pu-
mzi[#] ya midomo yake.^k

10:34 *Au "shoka." **11:4** *Au "uadili-
fu." #Au "roho."

SURA YA 10

a 2Nya 32:21
Isa 37:36

SURA YA 11

b Zb 132:11
Isa 53:2
Ufu 5:5
Ufu 22:16

c Ru 4:17
1Sa 17:58
Mt 1:1, 6
Lu 3:23, 32
Mdo 13:22, 23
Ro 15:12

d Yer 23:5
Yer 33:15
Zek 3:8
Zek 6:12

e Isa 42:1
Yoh 1:32
Mdo 10:38

f Lu 2:52

g Isa 9:6

h Ebr 5:7

i Yoh 7:24
Yoh 8:16

j Zb 2:9
Zb 110:2
Ufu 19:11, 15

k 2Th 2:8

Safu ya 2

a Ufu 3:14

b Isa 65:25

c Eze 34:25

d Ho 2:18

e Isa 2:4
Isa 35:9
Isa 60:18
Mik 4:4

f Isa 51:3
Isa 56:7
Isa 65:25

g Zb 22:27
Hab 2:14

h Ro 15:12
Ufu 22:16

i Mwa 49:10
Isa 49:22
Isa 62:10

j Mdo 11:18
Mdo 28:28

5 Uadilifu utakuwa mshipi
kiunoni mwake,
Na uaminifu mshipi wa
kiuno chake.^a

6 Mbwanawitu atakaa pamo-
ja na mwanakondoo kwa
muda fulani,^b

Na chui atalala pamoja na
mwanambuzi,

Na ndama na simba* na
mnyama aliyenoneshwa
wote watakuwa
pamoja;^{#c}

Na mvulana mdogo ata-
mwangoza.

7 Ng'ombe na dubu wataku-
la pamoja,
Na watoto wao watalala
pamoja.

Simba atakula majani
kama ng'ombe dume.^d

8 Na mtoto anayenyonya
atacheza juu ya shimo la
swila,

Na mtoto aliyeachishwa
kunyonya atatia mkono
wake juu ya shimo la
nyoka mwenye sumu.

9 Hawatasababisha ma-
dhara yoyote^e

Wala uharibifu wowote ka-
tika mlima wangu wote
mtakatifu,^f

Kwa maana kwa hakika
dunia itajaa ujuzi
kumhusu Yehova

Kama maji yanavyoifunika
bahari.^g

10 Siku hiyo mzizi wa Yese^h
utasimama kama ishara*
kwa ajili ya mataifa.ⁱ
Mataifa yatatafuta mwo-
ngozo kutoka kwake,^{#j}

11:6 *Au "mwanasimba mwenye manyo-
ya marefu shingoni." #Au labda, "Na
ndama na simba watakula pamoja."
11:10 *Au "nguzo ya ishara." #Au "Ma-
taifa yatamtafuta."

Na mahali pake pa kupumzikia patakuwa na utukufu.

11 Siku hiyo Yehova atauyoosha tena mkono wake, mara ya pili, ili kuwakomboa watu wake waliobaki kutoka Ashuru,^a kutoka Misri,^b kutoka Pathrosi,^c kutoka Kushi,^d kutoka Elamu,^e kutoka Shinarri,^f kutoka Hamathi, na kutoka katika visiwa vya bahari. **12** Atainua ishara* kwa ajili ya mataifa na kuwakusanya watu wa Israeli^g waliotawanywa, na watu wa Yuda waliotawanywa atawakusanya pamoja kutoka katika pembe nne za dunia.^h

13 Wivu wa Efraimu utakuwa umetoweka,ⁱ

Na wale wanaomwonyesha Yuda uadui wataangamizwa.

Efraimu hatamwonea Yuda wivu,

Wala Yuda hatamwonyesha Efraimu uadui.^j

14 Nao watashuka chini kwa ghafla kwenye mitere-mko ya* Wafilisti upande wa magharibi;

Wakiwa pamoja watawaporu watu wa Mashariki.

Watauonoosha mkono wao dhidi ya[#] Edomu^k na Moabu,^l

Na Waamoni watakuwa raia wao.^m

15 Yehova ataigawanya* ghuba ya[#] bahari ya Misriⁿ Na kuutikisa mkono wake juu ya ule Mto.^o

11:11 *Yaani, Babilonia. 11:12 *Au "nguzo ya ishara." 11:14 *Tnn., "bega la." #Au "Mamlaka yao itafika juu ya." 11:15 *Au labda, "ataikausha." #Tnn., "ulimi wa." ^Yaani, Mto Efrati.

SURA YA 11

a Isa 11:16

b Isa 27:13
Yer 44:28
Mik 7:12

c Yer 44:15

d Sef 3:10

e Da 8:2

f Isa 66:19

g Ezr 1:2, 3
Isa 49:22
Isa 62:10h Zb 147:2
Isa 66:20i 2Nya 30:1, 10
Yer 31:6j Yer 3:18
Eze 37:16, 19
Ho 1:11k Amo 9:11, 12
Oba 18

l Isa 25:10

m Yer 49:2

n Kut 14:22

o Mwa 15:18

Safu ya 2

a Isa 19:23
Isa 27:13
Isa 35:8
Isa 40:3
Isa 57:14
Yer 31:21

b Ezr 1:2, 3

SURA YA 12

c Kum 30:3
Zb 30:5
Zb 85:1
Zb 126:1
Isa 40:2
Isa 66:13

d Isa 45:17

e Isa 26:4

f Zb 118:14
Ho 1:7

g Isa 49:10

h 1Nya 16:8
Zb 105:1, 2

i Kut 15:2

Kwa pumzi* yake inayounguzua ataipiga katika vijito vyake saba,[#]

Naye atawafanya watu watembee na kuvuka wakiwa wamevaa viatu vyao.

16 Na kutakuwa na barabara kuu^a kutoka Ashuru kwa ajili ya watu wake waliobaki,^b

Kama ilivyokuwa kwa ajili ya Israeli siku aliyotoka nchini Misri.

12 Siku hiyo hakika utasema:

"Ninakushukuru, Ee Yehova,

Kwa maana ingawa ulinikasirikia,

Hasira yako ilipoa hatua kwa hatua, nawe ukani-fariji.^c

2 Tazama! Mungu ni wokovu wangu.^d

Nitamtumaini nami sitaogoga;^e

Kwa maana Yah* Yehova ni nguvu zangu na uwezo wangu,

Naye amekuwa wokovu wangu."^f

3 Mtateka maji kwa kushangilia

Kutoka kwenye chemchemi za wokovu.^g

4 Na siku hiyo mtasema:

"Mshukuruni Yehova, liitieni jina lake, Yajulisheni mataifa mateendo yake!^h

Tangazeni kwamba jina lake limekwezwa.ⁱ

11:15 *Au "roho." #Au labda, "ataipiga iwe mito saba." 12:2 *"Yah" ni ufupisho wa jina Yehova.

5 Mwimbieni sifa* Yehova^a kwa maana ametenda mambo makuu.^b
Jambo hilo na litangazwe duniani kote.

6 “Paza sauti na upige kelele kwa shangwe, ewe mkaaji* wa Sayuni, Kwa maana Mtakatifu wa Israeli ni mkuu katikati yako.”

13 Tangazo dhidi ya Babiloni,^c ambalo Isaya^d mwana wa Amози aliona katika maono:

2 “Simamisheni ishara*^e juu ya mlima wa miamba isiyo na kitu.

Wapazieni sauti, wapungieni mkono, Ili waingie katika milango ya watu wenye vyeo.

3 Nimewapa amri wale ambao nimewaweka rasmi.*^f

Nimewaita mashujaa wangu ili kuonyesha hasira yangu,

Watu wangu wanaoshangilia kwa majivuno.

4 Sikilizeni! Umati milimani; Ni kama sauti ya watu wengi sana!

Sikilizeni! Ghasia za falme,

Za mataifa yaliyokusanyika pamoja!^g

Yehova wa majeshi anakusanya jeshi kwa ajili ya vita.^h

5 Wanakuja kutoka nchi ya mbali,ⁱ

Kutoka mwisho wa mbingu,

12:5 *Au “Mpigieni muziki.” 12:6 *Tnn., “mkaaji wa kike.” Usemi huu unarejelea wakaaji wote kuwa kama mwanamke. 13:2 *Au “nguzo ya ishara.” 13:3 *Tnn., “watu wangu waliotakaswa.”

SURA YA 12

a Zb 149:3

b Zb 98:1

SURA YA 13

c Yer 25:12

Yer 50:1-3

Ufu 18:2

d Isa 1:1

e Yer 51:12

Yer 51:27, 28

f Isa 45:1

g Da 5:28

h Yer 50:15

i Yer 50:9

Yer 51:28

Safu ya 2

a Yer 51:11

b Isa 13:18

Yer 50:13

c Yer 50:43

d Da 5:6

e Yer 50:23, 29

f Ayu 9:9

Ayu 38:31

Amo 5:8

g Zb 137:8

Yer 51:37

Ufu 18:2

Yehova na silaha za ghadhabu yake,
Ili kuiangamiza dunia yote.^a

6 Ombolezeni kwa sauti, kwa maana siku ya Yehova iko karibu!

Itakuja kama maangamizi kutoka kwa Mweza-Yote.^b

7 Ndiyo maana mikono yote italegea,

Na moyo wa kila mwana-damu utayeyuka kwa woga.^c

8 Watu wameshikwa na wasiwasi.^d

Wanafurukuta na kushikwa na uchungu, Kama mwanamke anayezaa.

Wanatazamana kwa hofu, Wakiwa na nyuso zinazowaka kwa maumivu.

9 Tazama! Siku ya Yehova inakuja,

Ikiwa na ukali na ghadhabu na hasira inayowaka, Ili kuifanya nchi iwe kitucha kutisha,^e

Na kuwaangamiza wate nda dhambi wa nchi kutoka ndani yake.

10 Kwa maana nyota za mbinguni na makundi yake ya nyota*^f

Hazitatoa nuru yake;

Jua litakuwa na giza linapochomoza,

Nao mwezi hautatoa mwanga wake.

11 Nitaiadhibu* dunia inayokaliwa kwa sababu ya ubaya wake,^g

13:10 *Tnn., “na Kesili zao,” labda maneno haya yanarejelea kundi la nyota la Orioni na makundi mengine ya nyota yaliyo karibu. 13:11 *Au “Nitaiwajibisha.”

- Na waovu kwa sababu ya uovu wao.
Nitakikomesha kiburi cha wenye kimbelebele, Nami nitayashusha maji-vuno ya waonevu.^a
- 12** Nitamfanya mwanadamu anayeweza kufa kuwa haba kuliko dhahabu safi,^b
Na wanadamu kuwa haba kuliko dhahabu ya Ofiri.^c
- 13** Ndiyo maana nitazifanya mbingu zitetemeke
Na dunia itatikiswa itoke mahali pake^d
Kwa sababu ya ghadhabu ya Yehova wa majeshi katika siku ya hasira yake inayowaka.
- 14** Kama swala anayewindwa na kama kondoo wasio na mtu wa kuwakusanya
Kila mtu atarudi kwa watu wake mwenyewe;
Kila mtu atakimbilia nchi yake mwenyewe.^e
- 15** Yeyote atakayepatikana atachomwa kwa silaha,
Na yeyote atakayekamatwa atauawa kwa upanga.^f
- 16** Watoto wao wataavunjwa vipandevipande mbele ya macho yao,^g
Nyumba zao zitaporwa, Na wake zao watabakwa.
- 17** Tazama, ninawainua Wamedi dhidi yao,^h
Ambao hawaioni fedha kuwa kitu
Na ambao hawapendezwi na dhahabu.
- 18** Pinde zao zitawavunjavnja vijana;ⁱ
Hawatausikitikia uzao wa tumbo

SURA YA 13

a Yer 50:29
Da 5:22, 23

b Yer 50:30
Yer 51:3, 4

c 1Fa 10:11

d Yer 51:29

e Yer 50:16

f Yer 51:3, 4

g Zb 137:8, 9

h Isa 21:2
Yer 50:9
Yer 51:11
Da 5:30, 31

i Yer 50:14

Safu ya 2

a Isa 47:5
Da 4:30

b Isa 47:1

c Mwa 19:24, 25
Yer 50:40

d Yer 50:3, 13
Yer 51:29, 37
Ufu 18:21

e Ufu 18:2

f Yer 51:33

SURA YA 14

g Law 26:42

h Zek 1:17

i Kum 30:1-3
Isa 66:20
Yer 24:6
Eze 36:24

j Isa 56:6, 7
Isa 60:3
Zek 8:22, 23

k Isa 61:5
Zek 2:8, 9

Wala kuwahurumia wato.

- 19** Na Babiloni, ufalme wenye utukufu zaidi,^{*a}
Uzuri na fahari ya Wakaldayo,^b
Litakuwa kama Sodoma na Gomora yalipoangamizwa na Mungu.^c
- 20** Halitakaliwa kamwe, Wala halitakuwa makao ya watu kwa vizazi vyote.^d
Hakuna Mwarabu atakayepiga hema lake huko, Na hakuna wachungaji watakaopumzisha mifugo yao huko.
- 21** Viumbe wa jangwani watalala huko;
Nyumba zao zitajaa bundi-tai.
Mbuni watakaa huko,^e
Mbuzi wa mwituni* watarukaruka huko.
- 22** Wanyama wanaopiga mayowe watalia kwa sauti katika minara yake,
Na mbwamwitu katika majumba yake ya kifahari.
Wakati wake umekaribia, na siku zake hazitarefu-shwa."^f
- 14** Kwa maana Yehova atamwonyesha rehema Ya-kobo,^g naye atawachagua tena Waisraeli.^h Atawafanya waisi* katika nchi yao,ⁱ na wakaaji wageni watajiunga nao na kushikamana na nyumba ya Yakobo.^j **2** Na watu watawachukua na kuwaleta mahali pao wenyewe, na nyumba ya Israeli itawamiliki katika nchi ya Yehova wakiwa watumishi wa kiume na wa kike;^k nao wa-
- 13:19** *Au "pambo la falme." **13:21** *Au labda, "Na roho waovu walio kama mbuzi." **14:1** *Au "Atawapumzisha."

tawateka wale waliokuwa wamewateka, nao watawatiisha wale waliokuwa wakiwalazimisha kufanya kazi.*

3 Siku ambayo Yehova atakupumzisha kutokana na uchungu wako na kutokana na msukosuko wako na kutokana na utumwa mgumu uliowe kwa chini yake,^a **4** utaisema methali* hii dhidi ya mfalme wa Babiloni:

“Jinsi yule anayewalazimisha wengine kufanya kazi[#] alivyofikia mwisho wake!

Jinsi ukandamizaji ulivyo kwisha!^b

5 Yehova ameivunja fimbo ya waovu,

Gongo la watawala,^c

6 Yule anayewapiga watu kwa hasira kwa mapigo yasiyokoma,^d

Yule anayeyatiisha mataifa kwa hasira kwa mateso yasiyoisha.^e

7 Dunia nzima imepumzika sasa, haina usumbufu.

Watu wanapaza sauti kwa shangwe.^f

8 Hata miberoshi inakushangilia,

Pamoja na mierezi ya Lebanoni.

Inasema, “Tangu ulipoa nguka,

Hakuna mkataji wa miti anayekuja kutukata.’

9 Hata Kaburi* chini limevurugika

Ili likupokee utakapoingia. Kwa sababu yako, lina-waamsha wale waliokufa ambao hawana uwezo,

14:2 *Au “wasimamizi wao wa kazi.”

14:4 *Au “dhihaka.” [#]Au “msimamizi wa kazi.” 14:9, 11, 15 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 14

a Ezr 3:1
Ezr 9:8
Yer 30:10

b Yer 50:23

c Zb 125:3

d 2Nya 36:17
Yer 50:17

e Hab 1:6
Zek 1:15

f Zb 126:2
Isa 49:13
Yer 51:48
Ufu 18:20

Safu ya 2

a Ufu 18:22

b 2Nya 36:17
Yer 51:7
Eze 29:19
Da 5:18, 19

c Isa 47:7
Da 4:30

d Da 5:22, 23

Viongozi wote wa dunia wanaokandamiza.*

Linawafanya wafalme wote wa mataifa wasimame kutoka kwenye viti vyao vya ufalme.

10 Wote wanaanza kusema na kukuambia,

‘Je, wewe pia umedhoofika kama sisi?’

Je, umekuwa kama sisi?

11 Kiburi chako kimeshushwa chini mpaka Kaburini,*

Sauti ya vinanda vyako.^a

Funza wametandikwa chini yako kama kitanda, Na blanketi lako ni minyoo.’

12 Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni,

Ewe unayeng’aa, mwana wa mapambazuko!

Jinsi ulivyokatwa ukaa ngushwa duniani,

Wewe uliyeyashinda mataifa!^b

13 Ulisema moyoni mwako, ‘Nitapanda juu mbinguni.’^c

Nitakiinua kiti changu cha ufalme juu ya nyota za Mungu,^d

Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano,

Katika sehemu za mbali zaidi za kaskazini.^e

14 Nitaenda juu ya mawingu; Nitajifananiha na Aliye Juu Zaidi.’

15 Badala yake, utashushwa chini mpaka Kaburini,* Katika sehemu zenye kina zaidi za shimo.

16 Wale wanaokuona wataku-kodolea macho;

14:9 *Tnn., “Mbuzi dume wote wa dunia wanaokandamiza.”

e Zb 48:1, 2

- Watakuchunguza kwa makini, wakisema,
 'Je, huyu ndiye yule mtu aliyekuwa akiitikisa dunia,
 Aliyekuwa akizitetemesha falme,^a
- 17** Aliyeifanya dunia inayokaliwa iwe kama nyika
 Na kuyapindua majiji yake,^b
 Aliyekataa kuwaruhusu wafungwa wake waende nyumbani?'^c
- 18** Wafalme wengine wote wa mataifa,
 Naam, wote, wamelala chini katika utukufu,
 Kila mmoja katika kaburi lake* mwenyewe.
- 19** Lakini wewe, umetupwa bila kaburi,
 Kama chipukizi* lililochukiwa,
 Ukiwa umevishwa watu waliouawa kwa kuchomwa upanga,
 Wanaoshuka chini kwenye mawe ya shimoni,
 Kama mzoga uliokanyagiwa chini kwa miguu.
- 20** Hutaungana nao kaburini,
 Kwa maana uliiharibu nchi yako mwenyewe,
 Uliwaua watu wako mwenyewe.
 Uzao wa watenda maovu hautatajwa tena kamwe.
- 21** Tayarisheni ubao wa kuwachinja wanawe
 Kwa sababu ya hatia ya mababu zao,
 Ili wasiinue na kuimiliki dunia
 Na kuyajaza majiji yao katika nchi."

14:18 *Tnn., "nyumba yake." **14:19** *Au "tawi."

SURA YA 14

a Yer 51:25

b 2Fa 25:21
Isa 64:10

c 2Fa 24:12, 14
2Fa 25:11

Safu ya 2

a Isa 43:14
Yer 50:25
Yer 51:56

b Yer 51:62

c Isa 13:1, 21
Yer 50:35, 39
Ufu 18:2

d 2Nya 32:21, 22
Isa 30:31
Isa 31:8
Isa 37:36, 37

e Isa 10:24

f Zb 33:11
Met 19:21
Met 21:30
Isa 46:11

g 2Nya 20:5, 6
Isa 43:13

h 2Fa 16:20
2Nya 28:27

22 "Nitainuka dhidi yao,"^a asema Yehova wa majeshi.

"Nami nitafuta kabisa kuto-ka Babiloni jina na watu waliobaki na watoto na wazao,"^b asema Yehova.

23 "Nami nitamfanya kuwa makao ya nungunungu na eneo lenye umajimaji, nami nitamfagia kwa ufagio wa maangamizi,"^c asema Yehova wa majeshi.

24 Yehova wa majeshi amepa hivi:

"Kama nilivyokusudia, ndivyo itakavyotukia, Na kama nilivyoamua, ndivyo itakavyotimia.

25 Nitamponda Mwashuru katika nchi yangu

Nami nitamkanyaga-kanyaga kwenye milima yangu.^d

Nira yake itaondolewa juu yao,

Na mzigo wake utaondolewa juu ya bega lao."^e

26 Hili ndilo jambo lililola-muliwa* dhidi ya dunia yote,

Na huu ndio mkono ulionyooshwa^f dhidi ya mataifa yote.

27 Kwa maana Yehova wa majeshi ameamua,

Na ni nani anayeweza kuli-zuia?^f

Mkono wake umenyoo-shwa,

Ni nani anayeweza kuurudisha nyuma?^g

28 Katika mwaka ambao Mfalme Ahazi alikufa,^h

tangazo hili lilitolewa:

29 "Usishangilie, ewe Ufilisti, yeyote kati yenu,

14:26 *Tnn., "Hili ndilo shauri lililotolewa." ^aAu "ulio tayari kupiga."

Kwa sababu tu gongo la yule anayewapiga limevunjwa.

Kwa maana kwenye mzizi wa nyoka^a atatoka nyoka mwenye sumu,^b

Na uzao wake utakuwa nyoka wa moto arukaye.*

30 Huku wazaliwa wa kwanza wa watu wa hali ya chini wakila

Na maskini wakilala kwa usalama,

Nitauua mzizi wako kwa njaa kati,

Na haku kitakachobaki kwa-ko kitauawa.^c

31 Omboleza kwa sauti, ewe lango! Paza kilio, ewe jiji! Ninyi nyote mtavunjika moyo, ewe Ufilisti!

Kwa maana moshi unakuja kutoka kaskazini,

Na hakuna wavivu katika vikosi vyake.”

32 Watawajibuje wajumbe wa taifa lile?

Kwamba Yehova ameuweka msingi wa Sayuni,^d

Na kwamba watu wa hali ya chini kati ya watu wake watakimbilika ndani yake.

15 Tangazo dhidi ya Moabu:^e
Kwa sababu limeharibiwa kwa usiku mmoja, Jiji la Ari^f la Moabu lime-nyamazishwa.

Kwa sababu limeharibiwa kwa usiku mmoja, Jiji la Kiri^g la Moabu lime-nyamazishwa.

2 Amepanda mpaka kwenye Nyumba* na mpaka Diboni,^h

SURA YA 14

a 2Nya 26:3, 6

b 2Fa 18:1, 8

c Yer 47:1
Eze 25:16
Yoe 3:4
Amo 1:6-8
Sef 2:4
Zek 9:5

d Zb 48:1-3
Zb 87:1, 2
Zb 132:13, 14

SURA YA 15

e Yer 9:25, 26
Eze 25:11

f Hes 21:28
Kum 2:9

g 2Fa 3:24, 25
Yer 48:31

h Yer 48:18

Safu ya 2

a Yer 48:1

b Hes 21:30
Yos 13:15-17

c Kum 14:1

d Yer 48:36, 37

e Yer 48:38

f Hes 32:37
Isa 16:9

g Amu 11:20

h Mwa 13:10

i Yer 48:34

j Yer 48:3, 5

Kwenye mahali pa juu ili kulia.

Moabu inaombolezea Nebo^a na Medeba.^b

Kila kichwa kimenyolewa upara,^c ndevu zote zime-nyolewa.^d

3 Wamevaa nguo za magunia katika barabara zake.

Kwenye paa zao na katika viwanja vyao vya jiji, wote wanaomboleza kwa sauti;

Wanashuka chini wakilia.^e

4 Heshboni na Eleale^f wanalia kwa sauti;

Sauti yao inasikika mpaka Yahazi.^g

Ndiyo sababu watu wenye silaha wa Moabu wanae-ndelea kupaza sauti.

Anatetemeka.*

5 Moyo wangu unamlilia Moabu.

Wakimbizi wake wameki-ambia mpaka Soari^h na Eglath-shelishiya.ⁱ

Kwenye njia inayopanda kwenda Luhithi wanalia wakipanda;

Kwenye njia ya kwenda Horonaimu wanalia kwa sauti kwa sababu ya msiba.^j

6 Kwa maana maji ya Nimrimu yamekuwa ukiwa; Majani mabichi yamekauka,

Majani yamekwisha na hakuna chochote kibichi kilichobaki.

7 Ndiyo sababu wanabeba kilichobaki katika maghala yao na utajiri wao;

14:29 *Au “nyoka mwenye sumu anayeurukuka.” 15:2 *Au “Hekalu.”

15:4 *Au “Nafsi yake inatetemeka.”

Wanavuka bonde* la mie-rebi.

- 8 Kwa maana kilio kinasikika katika eneo lote la Moabu.^a

Maombolezo yanafika Eglaimu;

Maombolezo yanafika Beer-elimu.

- 9 Kwa maana maji ya Dimoni yamejaa damu, Nami nina mengi zaidi kwa ajili ya Dimoni: Simba kwa ajili ya watu wa Moabu wanaoponyoka Na kwa ajili ya wale wanaobaki nchini.^b

16 Pelekeni kondoo dume kwa mtawala wa nchi, Kutoka Sela kupitia nyikani

Mpaka kwenye mlima wa binti ya Sayuni.

- 2 Kama ndege aliyefukuzwa kwenye kiota chake,^c Ndivyo mabinti wa Moabu watakvayokuwa kwenye vivuko vya Arnoni.^d

- 3 “Toeni shauri, tekelezeni uamuzi.

Fanya kivuli chako cha adhuhuri kiwe kama usiku.

Wafiche waliotawanyika na usiwasaliti wale wanaokimbia.

- 4 Watu wangu waliotawanyika na wakae ndani yako, Ee Moabu.

Uwe maficho kwao kwa sababu ya mwangamizaji.^e

Mkandamizaji ataufikia mwisho wake, Uharibifu utafikia mwisho, Na wale wanaowakanyaga wengine wataangamia kutoka duniani.

SURA YA 15

a Yer 48:20

b 2Fa 17:25, 26

SURA YA 16

c Yer 48:19

d Hes 21:13

e Yer 48:8, 42

Safu ya 2

a 2Sa 7:16, 17

b Zb 45:6
Zb 72:1, 2
Isa 9:6, 7
Isa 32:1
Yer 23:5

c Yer 48:26, 29
Sef 2:9, 10

d Amo 2:1

e Isa 15:2
Yer 48:20

f 2Fa 3:24, 25

g Yos 13:15, 17

h Hes 32:37, 38
Yos 13:15, 19

i Yos 13:24, 25
Yer 48:32

j Isa 15:4
Yer 48:34

- 5 Kisha kiti cha ufalme kitaimarishwa kabisa katika upendo mshikamanifu.

Yule anayekikalia katika hema la Daudi atakuwa mwaminifu;^a

Atahukumu kwa haki na kutekeleza uadilifu upesi.”^b

- 6 Tumesikia kuhusu kiburi cha Moabu—ana kiburi sana^c—

Majivuno yake na kiburi chake na ghadhabu yake;^d

Lakini maneno yake matupu yatakuwa ya bure.

- 7 Basi Moabu atamwombolezea Moabu;

Wote wataomboleza.^e

Wale waliopigwa wataomboleza kwa sababu ya keki za zabibu kavu za Kir-haresethi.^f

- 8 Kwa maana matuta ya Heshboni^g yamenyauka.

Mzabibu wa Sibma,^h Watawala wa mataifa wameyakanyaga matawi yake mekundu sana;^{*}

Walikuwa wamefika mpaka Yazeri;ⁱ

Walikuwa wameenea mpaka nyikani.

Machipukizi yake yalikuwa yameenea mpaka baharini.

- 9 Hiyo ndiyo sababu nitaulilia mzabibu wa Sibma kama ninavyolilia Yazeri.

Machozi yangu yatakulowesha ewe Heshboni na Eleale,^j

Kwa sababu vigelegele vya matunda yako ya kia-

16:8 *Au “matawi yake yaliyojaa zabibu nyekundu.”

ngazi na vya mavuno yako vimekoma.*

- 10** Furaha na shangwe zimeondolewa katika shamba la matunda, Na hakuna nyimbo za shangwe au vigelegele katika mashamba ya mizabibu.^a

Anayekanyaga hakanyagi tena divai katika mashingi, Kwa maana nimekomesha vigelegele.^b

- 11** Ndiyo sababu nina msukosuko ndani yangu kwa ajili ya Moabu,^c Kama kinubi kinapopigwa, Na sehemu yangu ya ndani kabisa kwa ajili ya Kirahesethi.^d

12 Hata Moabu akijichosha mahali pa juu na kwenda kusali katika patakatifu pake, hatatimiza lolote.^e

13 Hilo ndilo neno ambalo Yehova alisema awali kuhusu Moabu. **14** Na sasa Yehova anasema: "Katika muda wa miaka mitatu, kama miaka ya kibarua,* utukufu wa Moabu utafedheheshwa kwa vurugu nyingi za kila aina, na wale watakaobaki watakuwa wachache sana na wanyonge."^f

- 17** Tangazo dhidi ya Damasko:^g

"Tazama! Damasko halitakuwa jiji tena, Nalo litakuwa rundo la magofu."^h

- 2** Majiji ya Aroeriⁱ yataachwa;

16:9 *Au labda, "Kwa sababu kelele za vita zimeshuka juu ya matunda yako ya kiangazi na mavuno yako." **16:14** *Au "iliyohesabiwa kwa uangalifu kama kibarua anavyofanya"; yaani, kwa miaka mitatu kamili.

SURA YA 16

a Yer 48:33

b Sef 2:9

c Isa 15:5
Yer 48:36

d Isa 15:1

e Yer 48:7, 35

f Isa 25:10
Yer 48:46, 47
Sef 2:9

SURA YA 17

g Yer 49:23
Zek 9:1

h 2Fa 16:8, 9
Isa 8:4
Amo 1:5

i Hes 32:34
Yos 13:15, 16
2Fa 10:32, 33

Safu ya 2

a 2Fa 17:6
Isa 7:8
Isa 28:1, 2
Ho 5:14

b 2Fa 16:8, 9

c Yos 15:8, 12
Yos 18:11, 16

d Kum 4:27
Kum 24:20

e 2Nya 31:1

f Ho 8:6, 11

Yatakuwa mahali ambapo mifugo italala Na hakuna yeyote atakayeiogopesha.

- 3** Majiji yenye ngome yatato-weka Efraimu,^a

Na ufalme kutoka Damasko;^b

Na wale wanaobaki wa Siria

Watakuwa kama utukufu wa Waisraeli,*^c asema Yehova wa majeshi.

- 4** "Siku hiyo utukufu wa Yakobo utafifia,

Na mwili wake wenye afya utakonda.*

- 5** Itakuwa kama mvunaji anapovuna nafaka iliyo shambani

Na mkono wake unapovuna masuke ya nafaka,

Kama mtu anayeokota masalio ya nafaka katika Bonde la* Refaimu.^c

- 6** Ni masalio tu yatakayobaki,

Kama mzeituni unapopi-gwa:

Ni zeituni mbili au tatu zilizoiva zinazobaki kwenye tawi refu zaidi,

Ni nne au tano tu kwenye matawi yanayozaa matunda,^d asema Yehova Mungu wa Israeli.

7 Siku hiyo mwanadamu atamtazama Muumba wake, na macho yake yatamtazama Mtakatifu wa Israeli. **8** Hatazitazama madhabahu,^e kazi ya mikono yake;^f naye hatazama kile ambacho vidole vyake vimetengeneza, iwe ni

17:3 *Tnn., "wana wa Israeli." **17:4** *Tnn., "mafuta ya nyama yake yatapungua." **17:5** *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

miti mitakatifu* au vinara vya uvumba.

- 9** Siku hiyo majiji yake yenye ngome yatakuwa kama mahali palipoachwa mwituni,^a Kama tawi lililoachwa mbele ya Waisraeli; Litakuwa ukiwa.
- 10** Kwa maana umemsaheu Mungu^b wa wokovu wako; Hukumkumbuka Mwamba^c wa ngome yako. Ndiyo sababu unapanda mashamba makubwa maridadi* Na kupanda humo chipukizi la mgeni.[#]
- 11** Mchana unalizingushia shamba lako ua kwa uangalifu, Asubuhi unachipusha mbegu zako, Lakini mavuno yatatoweka katika siku ya ugonjwa na maumivu yasiyoweza kuponywa.^d
- 12** Sikilizeni! Kuna vurugu za watu wengi, Walio na msukosuko kama wa bahari! Kuna kelele za mataifa, Ambao sauti yao ni kama mngurumo wa maji yenye nguvu!
- 13** Mataifa yatatoa sauti kama mngurumo wa maji mengi. Atayakemea, nayo yatakimbia mbali sana, Yakifukuzwa kama makapi ya milima mbele ya upepo Kama mchongoma unao-

17:8 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 17:10 *Au "yanayopendeza." #Au "mungu wa kigeni."

SURA YA 17

a Ho 10:14
Amo 3:11

b Zb 50:22
Ho 8:14

c Kum 32:4
2Sa 22:32

d Kum 28:30
Ho 8:7

Safu ya 2

SURA YA 18

a Isa 20:3, 4
Eze 30:4

b 2Nya 12:2, 3
2Nya 14:9
2Nya 16:8

peperushwa na* upepo wa dhoruba.

- 14** Jioni kuna tisho la ghafla. Kabla ya asubuhi hayapo tena.

Hilo ndilo fungu la wale wanaotupora

Na kura ya wale wanaotunyanyang'anya mali zetu.

- 18** Ole wa nchi ya wadudu wenye mabawa yanayovuma

Katika eneo la mito ya Ethiopia!^a

- 2** Inatuma wajumbe kupitia baharini,

Wanaovuka maji katika vyombo vya mafunjo, ikisema:

"Nendeni, enyi wajumbe wenye mbio,

Kwa taifa lenye watu warefu na walio na ngozi laini,*

Kwa watu wanaogopwa kila mahali,^b

Kwa taifa lenye nguvu, linaloshinda,[#]

Ambalo nchi yake imefagiliwa na mito."

- 3** Enyi wakaaji wote wa nchi nanyi wakaaji wa dunia,

Mtakachooni kitakuwa kama ishara* iliyo inuliwa juu ya milima,

Nanyi mtasikia sauti kama ya pembe inapopigwa.

- 4** Kwa maana Yehova alinia-mbia hivi:

"Nitaendelea kutulia na kutazama* mahali pangu palipofanywa imara,

17:13 *Au "mbaruti katika." 18:2 *Tnn., "taifa lenye watu waliochomoza juu na kusuguliwa." #Au "taifa lenye nguvu nyingi linaloyakanyaga mataifa mengine." 18:3 *Au "nguzo ya ishara." 18:4 *Au labda, "kutazama kutoka."

Kama joto linalometameta pamoja na mwangaza wa jua,

Kama wingu la umande katika joto la mavuno.

5 Kwa maana kabla ya mavuno,

Ua linapokamilika na kuwa zabibu inayoiva, Machipukizi yake yatakata kwa miundu

Vikonyo vitakatwa na kuondolewa.

6 Wote wataachwa waliwe na ndege wanaowinda wa milimani

Na wanyama wa duniani. Ndege wanaowinda watawala wakati wa kiangazi, Na wanyama wote wa dunia watawala wakati wa mavuno.

7 Wakati huo zawadi italetwa kwa Yehova wa majeshi,

Kutoka kwa taifa lenye watu warefu na walio na ngozi laini,*

Kutoka kwa watu wanaoogopwa kila mahali,

Kutoka kwa taifa lenye nguvu, linaloshinda,#

Ambalo nchi yake imefagiliwa na mito,

Mpaka mahali pa jina la Yehova wa majeshi, Mlima Sayuni.”^a

19 Tangazo dhidi ya Misri:^b

Tazama! Yehova amepanda juu ya wingu linaloenda kwa kasi, naye anakuja Misri.

Miungu ya ubatili ya Misri itatetemeka mbele zake,^c

SURA YA 18

a Isa 8:18
Isa 24:23

SURA YA 19

b Yer 25:17, 19
Eze 29:2
Yoe 3:19

c Kut 12:12
Yer 43:12
Yer 46:25
Eze 30:13

Safu ya 2

a Isa 19:11, 13

b Isa 8:19
Mdo 16:16
Ufu 18:23

c Isa 20:3, 4
Yer 46:25, 26
Eze 29:19

d Eze 30:12
Zek 10:11

e Kut 2:3

f Kum 11:10

g Eze 29:10

Na moyo wa Misri utayeyuka ndani yake.

2 “Nitawachochea Wamisri dhidi ya Wamisri,

Nao watapigana, Kila mmoja atapigana na ndugu yake na jirani yake,

Jiji litapigana na jiji, ufalme utapigana na ufalme.

3 Na roho ya Misri itakuwa na msukosuko ndani yake,

Nami nitavuruga mipango yake.^a

Watatafuta msaada kutoka kwa miungu ya ubatili, Kwa wachawi na kwa wanaowasiliana na roho na kwa wabashiri.^b

4 Nitaitia Misri mikononi mwa bwana aliye katili, Na mfalme mkali atawatawala,”^c asema Bwana wa kweli, Yehova wa majeshi.

5 Na maji ya bahari yatakaushwa,

Na mto utakauka na kuwa mkavu.^d

6 Na mito itanuka; Mifereji ya Nile ya Misri itapungua na kukauka.

Matete na mafunjo yatazoza.^e

7 Mimea iliyo kandokando ya Mto Nile, kwenye kinnywa cha Mto Nile,

Na ardhi yote iliyopandwa mbegu kandokando ya Nile^f itakauka.^g

Itapeperushwa mbali, nayo haitakuwepo tena.

8 Na wavuvi wataomboleza, Wale wanaotupa ndoano ndani ya Mto Nile wataomboleza,

18:7 *Tnn., “taifa lenye watu waliocho-moza juu na kusuguliwa.” ^aAu “taifa lenye nguvu nyingi linaloyakanyaga ma-taifa mengine.”

Na wale wanaotandaza
nyavu zao juu ya maji
watafungua.

- 9** Mafundi wa kitani kilicho-
chambuliwa^a

Na wafumaji wa vitambaa
vyeupe wataibishwa.

- 10** Wafumaji wake watapo-
ndwa;
Vibarua wote watahuzu-
nika.*

- 11** Wakuu wa Soani^b ni wapu-
mbavu.

Washauri wenye hekima
zaidi wa Farao wanatoa
ushauri usio wa busara.^c
Mnawezaje kumwambia
Farao:

“Mimi ni mzao wa watu we-
nye hekima,
Mzao wa wafalme wa
kale?”

- 12** Basi, wako wapi watu
wenu wenye hekima?^d

Acheni wawaambie kama
wanajua kile ambacho
Yehova wa majeshi
ameamua kuhusu
Misri.

- 13** Wakuu wa Soani wamete-
nda kwa upumbavu;
Wakuu wa Nofu^{*e} wamedan-
ganywa;

Wakuu wa makabila yake
wameipotisha Misri.

- 14** Yehova amemwagia
roho ya mvurugo;^f

Nao wameipotisha Misri
katika kila jambo inalofan-
yana,

Kama mlevi anavyogaagaa
kwenye matapishi yake.

- 15** Na Misri haitakuwa na
kazi yoyote ya kufanya,
Iwe ni kwa ajili ya kichwa

SURA YA 19

a Kut 9:25, 31
Met 7:16

b Zb 78:12
Eze 30:14

c Isa 44:25

d Mwa 41:8
Ifa 4:30
Mdo 7:22

e Yer 46:14
Eze 30:13

f Ayu 12:20, 24
Isa 19:3

Safu ya 2

a Isa 11:15

b Isa 20:3, 4
Yer 25:17, 19
Yer 43:10, 11
Eze 29:6

c Yer 43:4, 7
Yer 44:1

d Isa 19:1
Yer 46:13

e Isa 11:16
Isa 35:8
Isa 40:3

au mkia, chipukizi au
utete.*

16 Siku hiyo Misri itakuwa
kama wanawake, itateteme-
ka na kuogopa kwa sababu ya
mkono wenye kutisha ambao
Yehova wa majeshi anainua
dhidi yake.^a **17** Na nchi ya
Yuda itaifanya Misri iogope.
Watahofu kila mara Yuda ina-
potajwa kwa sababu ya uamu-
zi ambao Yehova wa majeshi
amefanya dhidi yao.^b

18 Siku hiyo kutakuwa na
majiji matano katika nchi
ya Misri yanayozungumza lu-
gha ya Kanaani^c na kuapa
kuwa washikamanifu kwa Ye-
hova wa majeshi. Jiji moja li-
taitwa Jiji la Kubomoa.

19 Siku hiyo kutakuwa na
madhabahu kwa ajili ya Yeho-
va katikati ya nchi ya Misri
na nguzo kwa ajili ya Yehova
kwenye mpaka wake. **20** Ita-
kuwa ishara na ushahidi kwa
Yehova wa majeshi nchini Mis-
ri; kwa maana watamlilia Ye-
hova kwa sauti kwa sababu ya
wakandamizaji, naye atawa-
pelekea mwokozi, aliye mkuu,
ambaye atawaokoa. **21** Na
Yehova atajulikana kwa Wam-
isri, na Wamisri watamjua
Yehova siku hiyo, nao wata-
toa dhabihu na zawadi na ku-
weka nadhiri kwa Yehova na
kuitimiza. **22** Yehova atai-
piga Misri,^d ataipega na kuipo-
nya; nao watamrudia Yehova,
naye atasikiliza maombi yao
ya kusihi na kuwaponya.

23 Siku hiyo kutakuwa na
barabara kuu^e kutoka Misri
kwenda Ashuru. Kisha Ashu-
ru itakuja Misri, na Misri itae-
nda Ashuru; na Misri itamtu-

19:10 *Au “watahuzunika katika nafsi.”
19:13 *Au “Memfisi.”

19:15 *Au labda, “tawi la mtende au
tete.”

mikia Mungu pamoja na Ashuru. **24** Siku hiyo Israeli itakuwa ya tatu pamoja na Misri na pamoja na Ashuru,^a baraka katikati ya dunia, **25** kwa maana Yehova wa majeshi atakuwa amewabariki, akisema: “Wabarikiwe watu wangu, Misri, na kazi ya mikono yangu, Ashuru, na urithi wangu, Israeli.”^b

20 Mwaka ambao Mfalme Sargoni wa Ashuru alituma Tartani* aende Ashdodi,^c alipigana na Ashdodi na kuliteka.^d **2** Wakati huo Yehova alisema hivi kupitia Isaya^e mwana wa Amози: “Nenda ukavue nguo ya magunia kutoka kiunoni mwako, na uvue viatu vilivyo miguuni mwako.” Naye akafanya hivyo, akatembea akiwa uchi* na bila viatu.

3 Kisha Yehova akasema: “Kama mtumishi wangu Isaya alivyotembea akiwa uchi na bila viatu kwa miaka mitatu ili kuwa ishara^f na dalili dhidi ya Misri^g na dhidi ya Ethiopia,^h **4** hivyo ndivyo mfalme wa Ashuru atakavyowaongoza mataka wa Misriⁱ na wahamisha wa Ethiopia, wavulana na wanaume wazee, wakiwa uchi na bila viatu na matako yakiwa wazi, uchi wa* Misri. **5** Nao wataogopa na kuona aibu kwa ajili ya Ethiopia tumaini lao na kwa ajili ya Misri fahari yao.* **6** Wakaa-ji wa eneo hili la pwani watasema siku hiyo, “Tazama kilicholipata tumaini letu, tulilolikimbilia ili kupata msaa-

20:1 *Au “kamanda.” 20:2 *Au “akiwa amevaa mavazi machache.” 20:4 *Au “aibu ya.” 20:5 *Au “Misri ambayo walivutiwa na urembo wake.”

SURA YA 19

a Zek 2:11

b Kum 32:9
Zb 115:12
Isa 61:9

SURA YA 20

c Yos 13:2, 3

d Amo 1:8

e Isa 1:1

f Isa 8:18

g Isa 19:1

h Isa 18:1

i Isa 19:4

Safu ya 2

SURA YA 21

a Isa 13:1, 20

b Isa 13:4, 18

c Yer 51:11, 28
Da 5:28, 30d Zb 137:1
Isa 14:4, 7
Isa 35:10

e Hab 3:16

f Da 5:1

da na kuokolewa kutoka kwa mfalme wa Ashuru! Tutaokokaje sasa?”

21 Tangazo dhidi ya nyika ya bahari:^{*a}

Msiba unakuja kama pepo za dhoruba zinazovuma kusini,

Kutoka nyikani, kutoka katika nchi inayotisha.^b

2 Nimeambiwa maono ya kutisha:

Mwenye hila anatenda kwa hila,

Na mwangamizaji, anaangamiza.

Nenda juu, ewe Elamu! Zingira, ewe Umedi!^c

Nitakomesha kilio chote cha uchungu alichosababisha.^d

3 Ndiyo sababu nina maumivu makali.^{*e}

Ninafurukuta kwa uchungu,

Uchungu kama wa mwanaumke anayezaa.

Nimetaabika sana hivi kwamba siwezi kusikia;

Nimesumbuka sana hivi kwamba siwezi kuona.

4 Moyo wangu unadundadunda; ninatetemeka kwa hofu.

Gizagiza la jioni nililotamani sana linanifanya nitetemeke.

5 Andaeni meza na mpange viti!

Mle na mnywe!^f

Simameni, enyi wakuu, itieni* ngao mafuta.

6 Kwa maana Yehova alinia-ambia hivi:

21:1 *Inaonekana kwamba usemi huu unarejelea eneo la Babilonia ya kale. 21:3 *Tnn., “kiuno changu kimejaa maumivu.” 21:5 *Au “ipakeni.”

“Nenda, mweke mlinzi na umwambie aseme yale anayoyaona.”

7 Naye akaona gari la vita pamoja na kundi la farasi,

Gari la vita la punda,
Gari la vita la ngamia.
Alitazama kwa makini,
akiwa amekaza fikira sana.

8 Kisha akaita kwa sauti kama simba:

“Ee Yehova, ninasimama daima juu ya mnara wa mlinzi wakati wa mchana,

Nami ninasimama katika kituo changu cha ulinzi kila usiku.^a

9 Tazama kinachokuja:

Wanaume wakiwa katika gari la vita na kundi la farasi wa vita!”^b

Kisha akasema:

“Ameanguka! Babiloni ameanguka!”^c

Sanamu zake zote za kuchongwa za miungu yake amezivunjavunja na kuziangusha chini!”^d

10 Enyi watu wangu walio-purwa,

Mazao ya* uwanja wangu wa kupuria,^e

Nimewaambia yale niliyosikia kutoka kwa Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli.

11 Tangazo dhidi ya Duma:*

Kuna mtu anayeniita kuto-ka Seiri:^f

“Mlinzi, kuna habari gani za usiku?

Mlinzi, kuna habari gani za usiku?”

21:10 *Tnn., “Mwana wa.” 21:11 *Maana yake “Kimya.”

SURA YA 21

a Eze 3:17
Hab 2:1

b Yer 50:3, 9
Yer 51:27, 28

c Isa 13:19
Isa 14:4
Isa 45:1
Yer 51:8
Da 5:28, 30
Ufu 14:8
Ufu 18:2

d Yer 50:2
Yer 51:44, 52

e Ifa 8:46

f Mwa 32:3
Kum 2:8
Zb 137:7

Safu ya 2

a Yer 25:17, 23

b Ayu 6:19
Yer 25:17, 23

c Mwa 25:13
Zb 120:5
Wim 1:5
Isa 42:11
Yer 49:28
Eze 27:21

SURA YA 22

d Yer 6:6

12 Mlinzi akasema:

“Asubuhi inakuja, na usiku pia.

Ikiwa mnataka kuuliza, ulizeni.

Njoooni tena!”

13 Tangazo dhidi ya jangwa tambarare:

Mtakaa usiku kucha msituni katika nchi tambarare ya jangwani,

Enyi misafara ya Dedani.^a

14 Leteni maji ili mkampokee mwenye kiu,

Enyi wakaaji wa nchi ya Tema,^b

Mleteeni mkate yule anayekimbia.

15 Kwa maana wamekimbia kwa sababu ya panga,

kwa sababu ya upanga uliochomolewa,

Kwa sababu ya upinde uliopindwa, na kwa sababu ya ukatili wa vita.

16 Kwa maana Yehova ali-niambia hivi: “Katika muda wa mwaka mmoja, kulingana na miaka ya kibarua,^{*} utukufu wote wa Kedari^c utafikia mwisho. **17** Wapiga upinde waliobaki kati ya mashujaa wa Kedari watakuwa wachache, kwa maana Yehova Mungu wa Israeli amesema hivyo.”

22 Tangazo kuhusu Bonde la Maono:^{*d}

Una tatizo gani hivi kwa-mba watu wako wote wamepanda juu ya paa?

2 Ulijaa machafuko, Jiji lenye msukosuko, mji wenye furaha.

21:16 *Au “iliyohesabiwa kwa uangalifu kama kibarua anavyofanya”; yaani, kwa mwaka mmoja kamili. 22:1 *Inaonekana maneno haya yanarejelea Yerusalemu.

Watu wako waliouawa ha-wakuuawa kwa upanga, Wala hawakufa vitani.^a

- 3 Madikteta wako wote wamekimbua pamoja.^b

Walichukuliwa kuwa wafungwa bila kutumia upinde.

Wote waliopatikana walichukuliwa kuwa wafungwa.^c

Ingawa walikuwa wamekimbilia mbali sana.

- 4 Ndiyo sababu nilisema:

“Msinitazame, Nami nitalia kwa uchungu.^d

Msisisitize kunifariji Kwa sababu ya kuangami-zwa kwa binti ya* watu wangu.^e

- 5 Kwa maana ni siku ya mvurugo na ya kushindwa na ya wasiwasi,^f

Kutoka kwa Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi,

Katika Bonde la Maono. Ukuta unabomolewa^g Na kuna kilio kwenye mlima.

- 6 Elamu^h inachukua podo Pamoja na magari ya vita yenye watu na farasi,* Na Kiriⁱ inafunua[#] ngao.

- 7 Mabonde yako yaliyo mazuri zaidi

Yatajaa magari ya vita, Na farasi* watajipanga lan-goni,

- 8 Na pazia la Yuda litaondolewa.*

22:4 *Tashihisi ya kishairi, ambayo labda inaonyesha sikitiko au huruma. 22:6, 7 *Au “wapanda farasi.” 22:6 #Au “inatayarisha.” 22:8 *Au “ulinzi wa Yuda utaondolewa.”

SURA YA 22

a Isa 3:1
Yer 38:2
Omb 4:9

b 2Fa 25:4, 5

c 2Fa 25:11

d Yer 4:19
Yer 8:18, 19
Yer 9:1

e Mik 1:8, 9

f Mik 7:4

g 2Fa 25:10
Ne 1:3

h Mwa 10:22

i 2Fa 16:9

Safu ya 2

a 1Fa 7:1, 2

b 2Fa 25:9, 10
Yer 52:7

c Ne 3:15

d Yoe 2:17

e Isa 5:12
Isa 56:12
Amo 6:1, 4
Lu 17:27
Yak 5:5

f 1Ko 15:32

g Law 26:31
Isa 1:11
Yer 15:1
Eze 24:13

h 2Fa 18:37
2Fa 19:2

“Siku hiyo utatazama kuelekea ghala la silaha la Nyumba ya Msitu,^a 9 nanyi mtayaona yale mashimo mengi yaliyo katika ukuta wa Jiji la Daudi.^b Nanyi mtayakusanya maji ya kidimbwi cha chini.^c 10 Mta-zihesabu nyumba za Yerusalemu, nanyi mtazibomoa nyumba hizo ili kuimarisha ukuta. 11 Nanyi mtatengeneza beseni kati ya hizo kuta mbili kwa ajili ya maji ya kidimbwi cha zamani, lakini hamtamtegemea Muumba* wake Mkuu, nanyi hamtamwona Yule aliyeibuni zamani.

12 Siku hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, Atawaambia watu walie na kuomboleza,^d Wanyoe vichwa na kuvaa nguo za magunia.

13 Lakini badala yake, kuna shehere na kushangilia, Kuchinja ng’ombe na kuchinja kondoo, Kula nyama na kunywa divai.^e ‘Acheni tule na tunywe, kwa maana kesho tutakufa.’^f

14 Kisha Yehova wa majeshi akajifunua masikioni mwangu: “Uovu huu hauta-funikwa kwa ajili yenu mpa-ka ninyi watu mtakapokufa,^g asema Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi.”

15 Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, anasema hivi: “Ingia kwa huyu msimamizi-nyumba, kwa Shebna,^h anayesimamia nyumba,* na umwambie, 16 ‘Una masilahi gani hapa, na je, una

22:11 *Au “Mtengenezaji.” 22:15 *Au “jumba la mfalme.”

mtu wako hapa hivi kwamba umejichimba kaburi hapa? Anachimba kaburi lake mahali palipoinuka; anajichongea mahali pa kupumzika* katika jabali. **17** "Tazama! Yehova atakutupa chini kwa nguvu, ewe mwanamume, na kukukamata kwa nguvu. **18** Hakika atakufunga kwa nguvu na kukurusha kama mpira katika nchi pana. Utafia huko, na huko magari yako yenye utukufu yatakuwa fedheha kwa nyumba ya bwana wako. **19** Nami nitakung'oa madarakani na kukufukuza kutoka katika cheo chako.

20 "Siku hiyo nitamwita mtumishi wangu Eliakimu^a mwana wa Hilkia, **21** nami nitamvisha kanzu yako na kumfunga kwa nguvu ukumbuu wako,^b nami nitatia mam-laka yako* mkononi mwake. Naye atakuwa baba kwa wakaaji wa Yerusalemu na nyumba ya Yuda. **22** Nami nitauweka ufunguo wa nyumba ya Daudi^c juu ya bega lake. Atafungua na hakuna yeyote atakayefunga; naye atafunga na hakuna yeyote atakayefungua. **23** Nitampigilia kama kigingi mahali panapodumu, naye atakuwa kama kiti cha ufalme cha utukufu kwa nyumba ya baba yake. **24** Nao watauning'iniza juu yake utukufu* wote wa nyumba ya baba yake, wazao na watoto,[#] vyombo vyote vidogo, vyombo vyenye umbo la bakuli, na pia mitungi yote mikubwa.

25 "Siku hiyo, asema Yehova wa majeshi, 'kigingi kili-

22:16 *Tnn., "makao." 22:21 *Au "milki yako." 22:24 *Tnn., "uzito." #Au "machipukizi."

SURA YA 22

a 2Fa 18:26, 37

b Mwa 41:41, 42
Est 8:15

c Ufu 3:7

Safu ya 2

a Isa 22:15, 17

SURA YA 23

b Yer 25:17, 22

Yer 47:4

Eze 26:3

Eze 27:2

Yoe 3:4

Amo 1:9, 10

Zek 9:3, 4

c 2Nya 9:21

Eze 27:25

d Mwa 10:2, 4

Yer 2:10

Eze 27:6

e Mwa 10:15

Eze 27:8

f Yer 2:18

g Eze 27:32, 33

Eze 28:4

h Yer 47:4

i Isa 19:1, 16

j Eze 27:35

Eze 28:19

chopigiliwa mahali panapodumu kitang'olewa,^a nacho kitakatwa na kuanguka, na mzi-go ulio juu yake utaanguka na kuharibika, kwa maana Yehova mwenyewe amesema hayo."

23 Tangazo kuhusu Tiro:^b
Ombolezeni kwa sauti, enyi meli za Tarshishi!^c

Kwa maana bandari imeharibiwa; haiwezi kuingiwa.

Wamefunuliwa habari kutoka katika nchi ya Kitimu.^d

2 Nyamazeni, enyi wakaaji wa pwani.

Wafanyabiashara kutoka Sidoni^e wanaovuka bahari wamekujaza.

3 Nafaka* ya Shihori[#] ilienda juu ya maji mengi,^f

Mavuno ya Nile, mapato yake,

Yalileta faida ya mataifa.^g

4 Ona aibu, Ee Sidoni, ngome ya bahari,

Kwa sababu bahari ime-sema:

"Sijapata uchungu wa kuzaa, nami sijazaa,

Wala sijalea vijana wa ki-me wala wa kike."^{*h}

5 Kama wakati waliposikia habari kuhusu Misri,ⁱ

Watu watateseka kwa sababu ya habari kuhusu Tiro.^j

6 Vukeni mpaka Tarshishi! Ombolezeni kwa sauti, enyi wakaaji wa pwani!

7 Je, hili ndilo jiji lenu lili-okuwa na furaha tangu

23:3 *Tnn., "Mbegu." #Yaani, kijito cha Mto Nile. 23:4 *Tnn., "mabikira."

kale, tangu nyakati zake za zamani?

Miguu yake ilikuwa iki-mpeleka nchi za mbali ili akae huko.

- 8** Ni nani ambaye ameamua jambo hili dhidi ya Tiro, Anayewavika watu mataji, Ambaye wafanyabiashara wake walikuwa wakuu, Ambaye wafanyabiashara wake waliheshimiwa duniani kote?^a
- 9** Yehova wa majeshi mwenyewe ameamua hivi, Kutia unajisi kiburi chake kwenye uzuri wake wote, Kuwafedhehesha wote walioheshimiwa duniani kote.^b
- 10** Vuka nchi yako kama Mto Nile, ewe binti ya Tarshishi. Hakuna tena kiwanda cha meli.^{*c}
- 11** Ameunyoosha mkono wake juu ya bahari; Amezitikisa falme. Yehova ameamuru ngome za Foinike ziangamizwe.^d
- 12** Naye anasema: “Hutafurahi tena,^e Ewe uliyekandamizwa, binti bikira wa Sidoni. Simama, vuka mpaka Kitimu.^f Hata huko hutapata utulivu.”
- 13** Tazama! Nchi ya Wakaldayo.^g Hawa ndio watu—haikuwa Ashuru^h—Walimfanya kuwa mahali pa wale wanaokaa jangwani. Wamesimamisha minara yao ya kuzingira;

SURA YA 23

a Eze 28:2

b Da 4:37
Yak 4:6

c Isa 23:1
Eze 26:14, 17

d Eze 26:5, 15

e Eze 26:13

f Eze 27:6

g Isa 13:19
Hab 1:6

h Isa 10:12
Nah 3:18
Sef 2:13

Safu ya 2

a Eze 26:8, 9

b Isa 23:1

c Yer 25:8, 11
Yer 27:3, 6

d Isa 60:5

SURA YA 24

e Isa 5:5
Yer 4:6
Eze 6:6

f 2Fa 21:13

g Kum 28:63, 64
Ne 1:8
Yer 9:16

Wameivua minara yake yenye ngome;^a

Na kumfanya awe magofu yanayoporomoka.

- 14** Ombolezeni kwa sauti, enyi meli za Tarshishi, Kwa maana ngome yenu imeharibiwa.^b

15 Siku hiyo Tiro litasahauliwa kwa miaka 70,^c sawa na muda wa* maisha ya mfalme mmoja. Mwishoni mwa miaka 70, Tiro litakuwa kama wimbo huu wa kahaba unavyosema:

- 16** “Chukua kinubi, lizunguke jiji, ewe kahaba uliyesahauliwa.

Piga kinubi chako kwa ustadi;

Imba nyimbo nyingi, Ili wakukumbuke.”

17 Mwishoni mwa miaka 70, Yehova atalikazia fikira Tiro, nalo litarudia malipo yake na kufanya ukahaba na falme zote za ulimwengu zilizo duniani. **18** Lakini faida yake na malipo yake yatakuwa kitu kitakatifu kwa Yehova. Hayatahifadhiwa wala kuwekwa akiba, kwa sababu malipo yake yatakuwa kwa ajili ya wale wanaokaa mbele za Yehova, ili wale na kushiba na kuvaa mavazi ya kifahari.^d

24 Tazama! Yehova anaifanya nchi* kuwa tupu na ukiwa.^e

Anaigeuza juu chini^{ff} na kuwatawanya wakaaji wake.^g

- 2** Kila mtu atapatwa na hali ileile:

Watu na pia kuhani, Mtumishi na bwana wake,

23:15 *Tnn., “siku za.” **24:1** *Au “dunia.” *Au “Anausokota uso wa dunia.”

23:10 *Au labda, “bandari.”

- Kijakazi na bimbubwa wake,
Mnunuzi na muuzaji,
Mkopeshaji na mkopaji,
Anayedai na anayedaiwa.^a
- 3** Nchi itafanywa kuwa tupu kabisa,
Itaporwa kabisa,^b
Kwa maana Yehova amesema neno hilo.
- 4** Nchi inaomboleza;^{*c} inadhooifika.
Nchi inayozaa inanyauka; inafifia.
Watu mashuhuri wa nchi wananyauka.
- 5** Nchi imechafuliwa na wakaaji wake,^d
Kwa maana wamezivunja sheria,^e
Wamebadili amri,^f
Na kuvunja agano linalodumu.^{*g}
- 6** Ndiyo sababu laana inaimeza nchi,^h
Na wakaaji wake wamehesabiwa kuwa na hatia.
Ndiyo sababu wakaaji wa nchi wamepungua,
Na watu wachache sana wamebaki.ⁱ
- 7** Divai mpya inaomboleza,^{*j} mzabibu unanyauka,^j
Na wote walio wachangamfu moyoni wanalia kwa uchungu.^k
- 8** Furaha ya matari imekoma;
Kelele za wanaosherehekea zimekoma;
Sauti ya furaha ya kinubi imekoma.^l
- 9** Wanakunywa divai bila wimbo,
Na kileo ni kichungu kwa wale wanaokinywa.

24:4, 7 *Au labda, "inakauka." 24:5 *Au "la kale."

SURA YA 24

a Eze 7:12, 13

b Law 26:31
Kum 29:28

c Yer 4:28
Omb 1:4

d Law 18:24
Hes 35:33, 34
ZNya 33:9
Yer 3:1
Yer 23:10, 11
Omb 4:13

e 2Fa 22:13
Da 9:5

f Mik 3:11

g Kut 19:3, 5
Kut 24:7
Yer 31:32
Yer 34:18-20

h Law 26:15, 16

i Kum 4:27
Kum 28:15, 62

j Yer 8:13
Yoe 1:10

k Isa 32:12

l Yer 7:34

Safu ya 2

a 2Fa 25:8-10

b Omb 5:15

c Isa 32:14
Yer 9:11
Omb 1:4
Omb 2:8, 9

d Kum 24:20

e Yer 6:9
Eze 6:8

f Isa 40:9
Yer 31:12
Yer 33:10, 11

g Isa 43:5

h Isa 11:11
Isa 60:9

i Kut 15:11
Ezr 9:15
Zb 145:7
Ufu 15:3

j Yer 9:2, 3

- 10** Mji uliohamwa umebomolewa kabisa;^a
Kila nyumba imefungwa ili mtu yeyote asiweze kuingia.
- 11** Wanalilia divai barabarani.
Kushangilia kote kumetoweka;
Shangwe ya nchi imetokomea.^b
- 12** Jiji limeachwa likiwa magofu;
Lango limevunjwawunjwa na kuwa rundo la kifusi.^c
- 13** Kwa maana hivi ndivyo itakavyokuwa katika nchi, miongoni mwa mataifa:
Kama mzeituni unapopi-gwa,^d
Kama masalio yanavyokusanywa baada ya mavuno ya zabibu kuisisha.^e
- 14** Watapaza sauti zao,
Watapiga vigelegele kwa shangwe.
Kutoka baharini* watatanga ngaza ukuu wa Yehova.^f
- 15** Ndiyo sababu watamtukuzia Yehova katika eneo la nuru;^{*g}
Katika visiwa vya bahari watalitukuza jina la Yehova Mungu wa Israeli.^h
- 16** Kutoka miisho ya dunia tunasikia nyimbo:
"Utukufu* kwa Aliye Mwa-dilifu!"ⁱ
Lakini ninasema: "Ninadhooifika, ninadhooifika!
Ole wangu! Wenye hila wametenda kwa hila;
Kwa hila wenye hila wametenda kwa hila."^j

24:14 *Au "magharibi." 24:15 *Au "mashariki." 24:16 *Au "Pambo."

17 Hofu na mashimo na mitogo inakusubiri, mkaaji wa nchi.^a

18 Yeyote anayeikimbia sauti inayotia hofu ataanguka shimoni,

Na yeyote anayetoka shimoni atanaswa na mtego.^b

Kwa maana malango ya mafuriko yaliyo juu yatafunguliwa,

Na misingi ya nchi itatetemeka.

19 Nchi imepasuka; Nchi imetikiswa; Nchi inafurukuta kwa fujo.^c

20 Nchi inapepesuka kama mlevi, Nayo inayumbayumba kama kibanda katika upepo.

Makosa yake yameilemea sana,^d

Nayo itaanguka, hivi kwa mba haitasimama tena.

21 Siku hiyo Yehova atalielekezea fikira zake jeshi lililo juu Na wafalme wa dunia walio duniani.

22 Nao watakusanywa pamoja Kama wafungwa waliokusanywa shimoni, Nao watafungiwa katika gereza lililo chini ya ardhi; Baada ya siku nyingi watakaziwa uangalifu.

23 Mwezi mpevu utafedhehesha, Na jua linalong'aa litaabishwa,^e Kwa maana Yehova wa majeshi amekuwa Mfalme^f

SURA YA 24

a Yer 8:3
Eze 14:21

b Yer 48:44

c Yer 4:24

d 2Fa 21:16
2Nya 36:15, 16
Yer 14:20

e Ufu 21:23

f Zb 97:1
Ufu 11:17

Safu ya 2

a Zb 132:13
Isa 12:6
Yoe 3:17
Mik 4:7
Zek 2:10

b 1Fa 8:11

SURA YA 25

c Zb 40:5
Zb 98:1
Zb 107:8
Zb 145:1, 4

d Zb 33:11

e Kum 32:4
Ne 9:33

f Zb 46:10
Zb 66:3
Eze 38:23

g Zb 46:1
Nah 1:7
Sef 3:12

h Zb 91:1
Zb 121:5-7
Isa 49:10

katika Mlima Sayuni^a na Yerusalemu Akiwa na utukufu mbele ya wazee wa watu wake.^{*b}

25 Ee Yehova, wewe ni Mungu wangu.

Ninakukweza, ninalisifu jina lako,

Kwa maana umetenda mambo yanayostaajabisha,^c

Mambo yaliyokusudiwa^{*} tangu nyakati za kale,^d Kwa uaminifu,^e kwa kutegemeka.

2 Kwa maana umelifanya jiji kuwa rundo la mawe, Mji wenye ngome kuwa magofu yanayoporumoka.

Mnara wa wageni si jiji tena;

Halitajengwa tena kamwe.

3 Ndiyo sababu watu wenye nguvu watakutukuza; Jiji la mataifa yenye uonevu litakuogopa.^f

4 Kwa maana umekuwa ngome kwa mtu wa hali ya chini,

Ngome kwa maskini katika taabu yake,^g

Kimbilio kutokana na dhoruba ya mvua,

Na kivuli wakati wa joto.^h

Wakati mlipuko wa waonevu ni kama dhoruba ya mvua inayopiga ukuta,

5 Kama joto katika nchi iliyokauka, Unazikomesha ghasia za wageni.

Kama joto linalokomesywa na kivuli cha wingu,

24:23 *Tnn., "mbele ya wazee wake."
25:1 *Au "Mashauri ya."

Ndivyo wimbo wa waonevu unavyonyamazishwa.

- 6** Katika mlima huu^a Yehova wa majeshi atawaandalia watu wa mataifa yote Karamu ya vyakula vinono,^b Karamu ya divai bora,^{*} Ya vyakula vinono vilivyojazwa urojorojo, Ya divai bora, iliyochujwa.
- 7** Katika mlima huu ataondoa^{*} kifuniko kina-chowafunika watu wote Na kifuniko kilichosokotwa[#] juu ya mataifa yote.
- 8** Atameza^{*} kifo milele,^c Na Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atafuta kabisa machozi katika nyuso zote.^d Shutuma ya watu wake ataiondoa katika dunia yote, Kwa maana Yehova mwenyewe amesema hayo.
- 9** Siku hiyo watasema: “Tazama! Huyu ndiye Mungu wetu!”^e Tumemtumaini yeye,^f Naye atatuokoa.^g Huyu ndiye Yehova! Tumemtumaini yeye. Na tufurahi na kushangilia katika wokovu wake.”^h
- 10** Kwa maana mkono wa Yehova utatulia juu ya mlima huu,ⁱ Na Moabu itakanyagwa-kanyagwa mahali pake^j Kama nyasi zinavyokanyagwa-kanyagwa na kuwa rundo la mbolea.

25:6 *Au “divai iliyowekwa kwenye machicha.” 25:7 *Tnn., “atameza.” #Au “shela iliyosokotwa.” 25:8 *Au “Ataondoa.”

SURA YA 25

a Isa 11:9
Isa 65:25

b Zb 72:16
Zb 85:11, 12
Yer 31:12

c Ho 13:14
1Ko 15:54
2Ti 1:10
Ufu 20:14

d Isa 35:10
Ufu 7:17
Ufu 21:4

e Isa 25:1

f Zb 37:34
Zb 146:5

g Mik 7:7

h Zb 20:5
Sef 3:14, 15

i Zb 132:13, 14
Isa 12:6

j Isa 15:1
Sef 2:9

Safu ya 2

a Yer 48:29
Yak 4:6

SURA YA 26

b Kut 15:1
2Sa 22:1
Isa 12:5

c Yer 33:10, 11

d Zb 48:2, 12

e Isa 60:18
Zek 2:4, 5

f Isa 60:11

g Zb 119:165
Isa 54:13
Flp 4:6, 7

h Zb 9:10
Yer 17:7

i 2Nya 20:20
Zb 62:8
Met 3:5

j Kum 32:4, 31

11 Atapigapiga mikono yake ndani yake

Kama mwogeleaji anavyopigapiga mikono yake ili kuogelea,

Naye atakishusha kiburi chake^a

Kwa mwendo stadi wa mikono yake.

12 Na jiji lenye ngome, pamoja na kuta zako ndefu za usalama,

Ataziangusha chini;

Atazibomoa na kuziangusha ardhini, mpaka mavumbini kabisa.

26 Siku hiyo wimbo huu utaimbwa^b katika nchi ya Yuda:^c

“Tuna jiji imara.^d

Anaufanya wokovu uwe kuta zake na maboma yake.^e

2 Fungueni malango^f ili taifa la uadilifu liingie, Taifa linalodumisha mwendo wa uaminifu.

3 Utawalinda wale wanaokutegemea kikamili;* Utawapa amani inayodumu,^g

Kwa sababu wanakutumaini wewe.^h

4 Mtumainini Yehova milele,ⁱ

Kwa maana Yah* Yehova ni Mwamba wa milele.^j

5 Kwa maana amewashusha chini wale wanaokaa juu, jiji lililo inuliwa.

Analiangusha chini, Analiangusha chini duniani;

Analitupa chini mavumbini.

26:3 *Au labda, “wale ambao mwelekeo wao hautikisiki.” 26:4 *“Yah” ni ufupisho wa jina Yehova.

- 6** Mguu utalikanyaga-kanyaga,
Miguu ya wanaoteseka,
nyayo za watu wa hali ya chini.”
- 7** Njia ya mwadilifu ime-nyooka.*
Kwa sababu wewe ni mnyoofu,
Utailainisha njia ya mwadilifu.
- 8** Tunapofuata njia ya hukumu zako, Ee Yehova,
Tumaini letu liko kwako.
Tunatamani* sana jina lako na ukumbusho wako.#
- 9** Usiku ninakutamani sana kwa nafsi yangu yote,
Naam, roho yangu inaendelea kukutafuta;^a
Kwa maana hukumu zina-
potoka kwako kwa ajili ya dunia,
Wakaaji wa nchi hujifunza kuhusu uadilifu.^b
- 10** Hata mwovu akionyeshwa kibali,
Hatajifunza uadilifu.^c
Hata katika nchi ya unyoo-
fu, atatenda uovu,^d
Naye hatauona ukuu wa Yehova.^e
- 11** Ee Yehova, mkono wako umeinuliwa, lakini hawauoni.^f
Wataona bidii yako kwa ajili ya watu wako na kuaibishwa.
Naam, moto uliokusudiwa maadui wako utawateke-
teza.
- 12** Ee Yehova, utatupatia amani,^g

26:7 *Au “ni tambarare.” 26:8 *Au “Kwa nafsi zetu tunatamani.” #Yaani, kwamba Mungu na jina lake likumbu-
kwe, litangazwe.

SURA YA 26

a Zb 63:6
Zb 119:62
Lu 6:12

b Zb 9:8
Zb 58:10, 11
Zb 85:11, 13
Zb 96:13
Zb 97:2
Isa 61:11

c Zb 106:43

d Yer 2:7
Ho 11:7

e Zb 28:5
Isa 5:12

f Isa 6:9

g Isa 57:19
Yer 33:6, 7

Safu ya 2

a 2Nya 12:7, 8

b 2Ti 2:19

c Yer 51:39

d Isa 60:21

e 1Fa 4:21

f Zb 78:34, 35
Ho 5:15

g Isa 25:8
Ho 13:14
Mk 12:26
Yoh 5:28, 29
Yoh 11:24, 25
Mdo 24:15
1Ko 15:21
1Th 4:14
Ufu 20:12, 13

Kwa sababu kila kitu ambacho tumefanya Ni wewe uliyetutumizia.

- 13** Ee Yehova Mungu wetu, mabwana wengine mbali na wewe wametutawala,^a Lakini tunalitaja jina lako peke yake.^b
- 14** Wamekufa; hawataishi. Hawana uwezo katika kifo, hawataamka.^c
Kwa maana umewaeleke-
zea fikira
Ili uwaangamize na kufu-
tilia mbali kabisa majina yao.
- 15** Umeongeza ukubwa wa taifa, Ee Yehova, Umeongeza ukubwa wa taifa;
Umejitukuza mwenyewe.^d
Umepanua sana mipaka yote ya nchi.^e
- 16** Ee Yehova, wakati wa taabu walikutafuta;
Walikumwagia sala yao kwa kunong’ona ulipo-
watia nidhamu.^f
- 17** Kama vile mwanamke mwenye mimba aliye ka-
ribu kuzaa
Anavyopata maumivu na kulia kwa uchungu,
Ndivyo hali yetu ilivyo kwa sababu yako, Ee Yehova.
- 18** Tulipata mimba, tulikuwa na maumivu ya kuzaa, Lakini ni kama tulikuwa tumeza upepo.
Hatujaleta wokovu nchini, Na hakuna mtu aliyezaliwa ili aishi nchini.
- 19** “Wafu wako wataishi. Maiti zangu zitaamka.*^g
Amkeni na mpige vigele-
gele kwa shangwe,

26:19 *Tnn., “Maiti yangu itaamka.”

Enyi mnaokaa mavu-
mbini!^a

Kwa maana umande wako
ni kama umande wa asu-
buhu,*

Na dunia itawaacha wale
waliokufa ambao hawana
uwezo wawe hai tena.[#]

- 20** Nendeni, watu wangu,
ingieni katika vyumba
vyenu vya ndani,
Na mfunge milango nyuma
yenu.^b
Jificheni kwa muda mfupi
Mpaka ghadhabu* itaka-
popita.^c

- 21** Kwa maana tazama! Ye-
hova anakuja kutoka
mahali pake
Ili kuwaita wakaaji wa nchi
wawajibike kwa sababu
ya uovu wao,
Na nchi itafunua umwagaji
wake wa damu
Nayo haitawafunika tena
watu wake waliouawa.”

- 27** Siku hiyo Yehova, aki-
wa na upanga wake
mkali na mkubwa na
wenye nguvu,^d
Atamwelekezea fikira Le-
wiathani,* yule nyoka
anayenyiririka,
Lewiathani, yule nyoka
anayepindapinda,
Naye atamuua mnyama
mkubwa sana aliye baha-
rini.

- 2** Siku hiyo mwimbieni hivi
huyo mwanamke:*
“Shamba la mizabibu la di-
vai inayotoa povu!^e

26:19 *Au labda, “umande wa mimea (miholi).” #Au “itawazaa wale waliokufa ambao hawana uwezo.” **26:20** *Au “shutuma.” **27:1** *Angalia Kamusi, uku. 2012. **27:2** *Inaonekana ni Israeli, hapa anarejelewa kuwa mwanamke na kufananishwa na shamba la mizabibu.

SURA YA 26

a Mwa 3:19

b Mwa 7:15, 16
Kut 12:22, 23
Met 18:10

c Zb 27:5
Zb 91:4

SURA YA 27

d Kum 32:41
Yer 47:6

e Zb 80:8
Isa 5:1
Yer 2:21

Safu ya 2

a Kum 33:29

b Isa 35:6
Isa 41:18
Isa 58:11

c Zb 121:4
Isa 46:3, 4

d Zb 85:2, 3
Isa 12:1

e Eze 39:25
Ho 14:5

f Isa 60:21, 22
Yer 30:18, 19

g Yer 4:11
Eze 13:13

h Isa 4:4
Isa 48:10

- 3** Mimi, Yehova, ninamli-
nda.^a
Kila wakati ninammwagi-
lia maji.^b
Ninamlinda usiku na
mchana,
Ili mtu yeyote asimdhuru.^c
- 4** Mimi sina ghadhabu.^d
Ni nani atakayenikabili
kwa vichaka vya miiba
na magugu katika vita?
Nitavikanyaga-kanyaga na
kuvichoma moto vyote
pamoja.
- 5** La sivyo, na ashikilie ngo-
me yangu kwa nguvu,
Na afanye amani pamoja
nami;
Acheni afanye amani pa-
moja nami.”
- 6** Siku zinazokuja Yakobo
atatia mizizi,
Israeli atachanua maua na
kuchipuka,^e
Nao watajaza mazao kati-
ka nchi.^f
- 7** Je, ni lazima apigwe kwa
pigo la yule anayempiga?
Au, je, ni lazima auawe
kama watu wake wali-
vyouawa?
- 8** Utashindana naye kwa
mlio wa kushtua utaka-
pokuwa ukimfukuza.
Atamfukuza kwa mlipuko
wake mkali katika siku
ya upepo wa mashariki.^g
- 9** Basi kwa njia hii uovu wa
Yakobo utafunikwa,^h
Na haya ndiyo yatakayoku-
wa mazao kamili dhambi
yake itakapoondolewa:
Atayafanya mawe yote ya
madhabahu
Yawe kama mawe ya cho-
kaa yaliyopondwa na
kuwa ungaunga,

Na hakuna miti mitakafifu* au vinara vya uvumba vitakavyobaki.^a

10 Kwa maana jiji lenye ngome litaachwa tupu;

Malisho yataachwa na kubaki kama nyika.^b

Ndama atalisha humo na kulala humo

Naye atakula matawi yake.^c

11 Vitawi vyake vitakapokauka,

Wanawake watakuja kuvivunja,

Na kuvitumia kuwasha moto.

Kwa maana watu hawa hawana uelewaji.^d

Ndiyo sababu Muumba wao hatawaonyesha rehema,

Na Yule aliyewaumba hatawaonyesha kibali.^e

12 Siku hiyo Yehova atayapiga kabisa matunda kuanzia kijito kinachotiririka cha ule Mto^f mpaka kwenye Korongo* la Misri,^f nanyi mtakusanywa mmoja baada ya mwingine, enyi watu wa Israeli.^g

13 Siku hiyo pembe kubwa itapigwa,^h na wale wanaoangamia katika nchi ya Ashuruⁱ na wale waliotawanywa katika nchi ya Misriⁱ watakuja na kumwinamia Yehova kwenye mlima mtakatifu huko Yerusalem.^k

28 Ole kwa taji* la kujionyesha[#] la walevi wa Efraimu^l

Na ua linalonyauka la uzuri wake wenye utukufu, Lililo kwenye kichwa cha

27:9, 12 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 27:12 [#]Yaani, Mto Efrati. 28:1 *Inaonekana neno hili linarejelea jiji kuu, Samaria. 28:1, 3 [#]Au "majivuno; kiburi."

SURA YA 27

a Mik 5:13, 14

b Isa 6:11, 12
Yer 26:18
Omb 2:5
Eze 36:4

c Isa 32:14

d Kum 32:28
Isa 1:3
Yer 4:22
Ho 4:6

e 2Nya 36:15, 16
Eze 9:9, 10

f Hes 34:2, 5

g Kum 30:3
Ne 1:9
Isa 11:11, 12
Amo 9:14

h Isa 49:22
Isa 62:10

i 2Fa 17:6
Isa 11:16
Ho 9:3

j Yer 43:4, 7
Zek 10:10

k Isa 2:3
Isa 25:6
Isa 52:1
Yer 3:17

SURA YA 28

l Isa 7:2

Safu ya 2

a 2Fa 17:6
Isa 17:3

b Isa 11:16

c Zb 18:34
Zb 68:35

bonde lenye rutuba la wale waliolemewa na divai!

2 Tazama! Yehova ana mtu mwenye nguvu na hodari.

Kama dhoruba ya mvua ya mawe yenye mngurumo, dhoruba ya upepo inayoharibu,

Kama dhoruba yenye mngurumo ya mafuriko yenye nguvu, Atalitupa chini kwa nguvu duniani.

3 Mataji ya kujionyesha[#] ya walevi wa Efraimu Yatakanyiwa chini kwa miguu.^a

4 Na ua linalonyauka la uzuri wake wenye utukufu Lililo juu ya kichwa cha bonde lenye rutuba, Litakuwa kama tini ya mapema kabla ya wakati wa kiangazi.

Mtu anapoiona, huimeza mara tu inapokuwa mkononi mwake.

5 Siku hiyo Yehova wa majeshi atakuwa taji la utukufu na shada maridadi kwa watu wake waliobaki.^b **6** Naye atakuwa roho ya haki kwa yule anayeketi katika hukumu na chanzo cha nguvu kwa wale wanaozuia mashambulizi lanngoni.^c

7 Na hawa pia wanapotea njia kwa sababu ya divai; Wanapepesuka kwa sababu ya vileo vyao.

Kuhani na nabii wanapotea njia kwa sababu ya kileo;

Divai inawavuruga, Nao wanapepesuka kwa sababu ya kileo chao;

Maono yao yanawafanya wapotee njia, Nao wanajikwaa wanapohukumu.^a

8 Kwa maana meza zao zimejaa matapishi machafu —Yamejaa kila mahali.

9 Mtu atamfundisha nani ujuzi, Na mtu atamfananulia nani ujumbe?

Je, ni wale walioachishwa kunyonya hivi karibuni, Wale walioondolewa kwenye matiti hivi karibuni?

10 Kwa maana ni “amri baada ya amri, amri baada ya amri, Mstari kwa mstari, mstari kwa mstari,^{*b} Hapa kidogo, pale kidogo.”

11 Kwa maana atazungu-mza na watu hawa kupitia watu wenye kigugumizi* na kwa lugha ya kigeni.^c **12** Alikuwa amewaambia: “Hapa ndipo mahali pa kupumzika. Yule aliyechoka na apumzike; hapa ndipo mahali pa kuburudika,” lakini walikataa kusikiliza.^d

13 Basi neno la Yehova litakuwa kwao:

“Amri baada ya amri, amri baada ya amri, Mstari kwa mstari, mstari kwa mstari,^{*e}

Hapa kidogo, pale kidogo,” Ili wanapotembea, Wajikwae na kuanguka nyuma

Na wavunjike na kunaswa na kukamatwa.^f

28:10, 13 *Au “Kamba ya kupimia juu ya kamba ya kupimia, kamba ya kupimia juu ya kamba ya kupimia.” **28:11** *Tnn., “midomo yenye kigugumizi.”

SURA YA 28

a 2Fa 16:10, 11
Yer 5:31

b 2Fa 21:13
Isa 28:17
Omb 2:8

c Kum 28:49, 50
Yer 5:15
1Ko 14:21

d Zb 81:10, 11

e Isa 28:17

f 2Nya 36:15, 16
Isa 8:14, 15

Safu ya 2

a Isa 28:18

b Isa 30:9, 10

c Zb 118:22

d Mt 21:42
Mk 12:10
Lu 20:17
Mdo 4:11

e Efe 2:19, 20

f Ro 9:33
Ro 10:11
1Pe 2:4, 6

g 2Fa 21:13

h Yer 11:20

i Isa 28:15

14 Basi sikieni neno la Yehova, ninyi mnaojigamba, Enyi watawala wa watu hawa wa Yerusalemu,

15 Kwa maana ninyi watu mnasema:

“Tumefanya agano na Kifo,^a

Na tumefanya mapatano* na Kaburi.[#]

Mafuriko makubwa ya ghafla yatakapopita,

Hayatatufikia,

Kwa maana tumeufanya uwongo kuwa kimbilio letu

Nasi tumejificha katika udanganyifu.”^b

16 Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Tazama, ninaweka jiwe lililojaribiwa liwe msingi katika Sayuni,^c

Jiwe la pembeni lenye thamani^d la msingi imara.^e

Hakuna yeyote anayeonyesha imani atakayeshikwa na wasiwasi.^f

17 Nami nitaifanya haki kuwa kamba ya kupimia^g

Na uadilifu utakuwa kifaa cha kusawazishia;^{*h}

Na mvua ya mawe itafagilia mbali kimbilio la uwongo,

Na maji yatafurika mahali pa kujificha.

18 Agano mlilofanya na Kifo litavunjwa,

Na mapatano yenu na Kaburi[#] hayatasimama.ⁱ

28:15 *Au labda, “tumetekeleza maono.” **28:15, 18** *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. **28:17** *Au “timazi.”

Mafuriko makubwa ya ghafla yatakapopita, Yatawaponda ninyi.

- 19** Kila mara yanapopita, Yatawafagilia mbali;^a Kwa maana yatapita asubuhi baada ya asubuhi, Mchana na usiku. Ni hofu tu itakayowafanya waelewe walichosikia.”^{*b}
- 20** Kwa maana kitanda ni kifupi sana mtu asiweze kujinyoosha juu yake, Na shuka iliyofumwa ni nyembamba sana isiweze kumfunika mtu.
- 21** Kwa maana Yehova atasimama kama katika Mlima Perasimu, Atainuka kama katika bonde lililo^{*} karibu na Gibeoni,^b Ili afanye tendo lake —tendo lake la ajabu— Na ili afanye kazi yake —kazi yake isiyo ya kawaida.^c
- 22** Sasa msidhihaki,^d Ili vifungo vyenu visikazwe zaidi, Kwa maana nimesikia kutoka kwa Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, Kwamba maangamizi yamekusudiwa kuipata nchi yote.^{*e}
- 23** Tegeni sikio, muisikilize sauti yangu; Kazeni fikirira na msikilize ninachosema.
- 24** Je, mkulima huendelea kulima mchana kutwa kabla hajapanda mbevu?

28:19 *Au labda, “Watakapoelewa, watahikwa na hofu kubwa.” **28:21** *Au “nchi tambarare ya chini iliyo.” **28:22** *Au “kuipata dunia yote.”

SURA YA 28

a Isa 24:1

b Yos 10:8-14
2Sa 5:20
1Nya 14:10-16c Omb 2:15
Hab 1:5-7d 2Nya 36:15, 16
Yer 20:7e Isa 10:23
Isa 24:1

Safu ya 2

a Zb 30:5
Zb 103:9
Mik 7:18b Kut 9:31, 32
Eze 4:9

c Zb 119:71

d Isa 41:15
Amo 1:3e Zb 103:9
Isa 21:10
Mik 7:18f Law 26:44
Yer 10:24g Zb 40:5
Yer 32:19
Ro 11:33

Je, huendelea kuyagongagonga mabonge ya udongo na kusawazisha shamba lake?^a

- 25** Baada ya kusawazisha ardhi, Je, hatawanyi jira na kupanda bizari, Na je, hapandi ngano, mtaama, na shayiri mahali pake Na kusemethi^b kwenye mipaka?
- 26** Kwa maana Yeye humfundisha^{*} njia inayofaa; Mungu wake humfundisha.^c
- 27** Kwa maana jira hai-sagwi kwa kifaa cha kupuria,^d Na gurudumu la gari la kukokotwa halizungushwi juu ya bizari. Badala yake, jira hupigwa kwa fimbo, Na bizari kwa gongo.
- 28** Je, mtu huiponda nafaka ili apate mkate? Hapana, haendelei kupura mfululizo;^e Na anapozungusha gurudumu la gari lake la kukokotwa juu yake akiwa na farasi wake, Yeye haipondi.^f
- 29** Na haya pia yanatoka kwa Yehova wa majeshi, Ambaye shauri^{*} lake lina-staajibisha Na ambaye ametimiza mambo makuu.^{*g}

28:26 *Au “humtia nidhamu kwa; humwadhibu kwa.” **28:29** *Au “kusudi.”^{*} Au “ambaye hekima yake inayotumika ni kuu.”

29 “Ole kwa Arieli, * Arieli, jiji ambalo Daudi alipiga kambi ndani yake!^a

Endelea mwaka baada ya mwaka;
Mzunguko wa sherehe^b na uendeleo.

2 Lakini nitaliletea taabu Arieli,^c
Na kutakuwa na kilio na maombolezo,^d
Nalo litakuwa kwangu kama jiko la madhabahu ya Mungu.^e

3 Nitapiga kambi pande zote dhidi yako,
Nami nitakuzingira kwa ngome
Na kujenga maboma dhidi yako.^f

4 Utashushwa chini;
Utazungumza kutoka ardhini,
Na mambo utakayosema yatakuwa mning’ono kwa sababu ya mavumbi.

Sauti yako itatoka ardhini^g
Kama sauti ya mtu anayewasiliana na roho,
Na maneno yako yatatoka mavumbini kama sauti ya ndege.

5 Umati wa maadui wako* utakuwa kama ungaunga laini,^h

Umati wa waonevu kama tu makapi yanayopeperuka.ⁱ

Na jambo hilo litatokea haraka, ghafla.^j

6 Yehova wa majeshi atawakazia fikira
Kwa mngurumo na tete-

29:1 *Huenda jina hili linamaanisha “Jiko la Madhabahu ya Mungu,” inaelekea ni Yerusalemu. **29:5** *Tnn., “wage-ni wako.”

SURA YA 29

a 2Sa 5:7, 9

b Kum 16:16

c Kum 28:53-55

d Isa 51:19
Omb 1:4

e Yer 15:14
Sef 1:7

f 2Fa 24:11
2Fa 25:1

g Isa 51:23

h Isa 13:19
Isa 14:22
Isa 21:9

i Isa 13:11
Isa 17:13

j Isa 47:9
Isa 48:3

Safu ya 2

a 1Sa 2:10
Yer 50:25
Nah 1:3

b Yer 25:12, 14

c Isa 10:12
Yer 51:24

d Hab 1:5

e Isa 6:9

f Isa 6:10
Ro 11:8

g Yer 14:14
Yer 27:15

h Mik 3:7

meko la ardhi na kelele kubwa,

Kwa upepo wa dhoruba na tufani na miali ya moto unaoteketeza.”^a

7 Kisha umati wa mataifa yote yanayopigana vita na Arieli^b

—Wale wote wanaopigana vita naye,

Minara inayomzingira,
Na wale wanaomsababishia taabu—

Watakuwa kama ndoto, maono ya usiku.

8 Naam, itakuwa kama mtu aliye na njaa anayeota kwamba anakula,

Lakini anaamka akiwa na njaa,*

Na kama mtu mwenye kiu anayeota kwamba anakunywa,

Lakini anaamka akiwa amechoka na akiwa na kiu.[#]

Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa umati wa mataifa yote

Yanayopigana vita dhidi ya Mlima Sayuni.^c

9 Pigweni na butwaa na mshangae;^d

Jipofusheni na mpofushwe.^e

Wamelewa, lakini si kwa divai;

Wanapepesuka, lakini si kwa sababu ya kileo.

10 Kwa maana Yehova amewamwagia roho ya usingizi mzito;^f

Ameyafunga macho yenu, enyi manabii,^g

Naye amefunika vichwa vyenu, enyi waonaji.^h

29:8 *Au “nafsi yake ikiwa tupu.” [#]Au “nafsi yake ikiwa imekauka.”

11 Maono yote yamekuwa kwenu kama maneno ya kitabu ambacho kimefungwa kwa muhuri.^a Wakimpa mtu anayejua kusoma na kumwambia: “Tafadhali, kisome kwa sauti,” atasema: “Siwezi, kwa maana kimefungwa kwa muhuri.” **12** Na wakimpa kitabu hicho mtu asiyejua kusoma na kumwambia: “Tafadhali, kisome kitabu hiki,” atasema: “Sijui kusoma hata kidogo.”

13 Yehova anasema: “Watu hawa hunikaribia kwa vinywa vyao Nao huniheshimu kwa miodomo yao,^b Lakini mioyo yao iko mbali sana nami; Na hofu yao kunielekea inategemea amri za wanadamu ambazo wamefundishwa.^c

14 Kwa hiyo, mimi Ndiye nitakayewatendea tena watu hawa mambo ya ajabu,^d Maajabu juu ya maajabu; Na hekima ya watu wao wenye hekima itato-weka, Na uelewaji wa watu wao wenye busara utafichwa.”^e

15 Ole wao wanaojitahidi sana kumficha Yehova mipango yao.^{*f} Wanatenda matendo yao mahali penye giza, Huku wakisema: “Ni nani anayetuona? Ni nani anayejua kutuhusu?”^g

16 Jinsi mnavyopotosha mambo!^{*}

29:15 *Au “shauri lao.” 29:16 *Au “Jinsi mlivyopotokal!”

SURA YA 29

a Isa 8:16

b Isa 48:1
Yer 5:2c Mt 15:7-9
Mk 7:6-8d Isa 28:21
Hab 1:5e Yer 8:9
1Ko 1:19

f Isa 30:1

g Eze 8:12

Safu ya 2

a Isa 64:8

b Yer 18:6

c Ro 9:20, 21

d Isa 35:1
Isa 41:19

e Isa 32:14, 15

f Isa 35:5
Isa 42:16

g Isa 41:16

h Mik 2:1

i Amo 5:10

j Eze 13:19

Je, mfinyanzi anapaswa kuonwa kuwa sawa na udongo?^a

Je, kitu kilichotengenezwa kinapaswa kusema kuhusu yule aliyekitengeneza: “Hakunitengeneza?”^b

Na je, kitu kilichotengenezwa kinasema kuhusu yule aliyekitengeneza: “Hana uelewaji?”^c

17 Katika muda mfupi, Lebanoni itageuzwa kuwa shamba la matunda,^d Na shamba hilo la matunda litaonwa kuwa msitu.^e

18 Siku hiyo viziwi watasikia maneno ya kile kitabu, Na kutoka katika utusitusi na giza macho ya vipofu yataona.^f

19 Wapole watashangilia sana katika Yehova, Na maskini miongoni mwa watu watashangilia katika Mtakatifu wa Israeli.^g

20 Kwa maana mwonevu hatakuwapo tena, Anayejigamba ataangamia, Na wote wanaokaa macho ili kusababisha madhara wataangamizwa,^h

21 Wale ambao kwa neno la udanganyifu wanawafanya wengine wawe na hatia, Wanaotega mitego ili kumnsasa mtetezi* katika lango la jiji,ⁱ Na wale ambao kwa ma-shtaka yasiyo na msingi humnyima haki mwadilifu.^j

29:21 *Tnn., “anayekaripia.”

22 Basi Yehova, aliyemko-mboa Abrahamu,^a anaiambia hivi nyumba ya Yakobo:

“Yakobo hataona aibu tena,

Na uso wake hautabadilika rangi tena.”^b

23 Kwa maana anapowaona watoto wake,

Ambao ni kazi ya mikono yake, katikati yake,^c

Watalitakasa jina langu; Naam, watamtakasa Mta-

katifu wa Yakobo, Nao watamwogopa Mungu

wala Israeli.^d

24 Wale waliopotoka rohoni watapata uelewaji,

Na wale wanaolalamika watakubali mafundisho.”

30 “Ole wao wana wakaidi,”^e asema Yehova,

“Wanaotekeleza mipango ambayo si yangu,^f

Wanaofanya miungano,^{*} lakini si kwa roho yangu,

Ili kuongeza dhambi juu ya dhambi.

2 Wanashuka kwenda Misri^g bila kuniomba ushauri,^h

Ili kupata usalama chini ya ulinzi wa Farao[#]

Na kupata kimbilio katika kivuli cha Misri!

3 Lakini ulinzi wa Farao utawaletea aibu,

Na kukimbilia katika kivuli cha Misri kutawaletea fedheha.ⁱ

4 Kwa maana wakuu wake wako Soani,^j

29:22 * Yaani, kwa sababu ya aibu na kukata tamaa. 30:1 * Tnn., “wanaomwaga sadaka ya kinywaji,” inaonekana inarejelea kufanya mapatano. 30:2 * Au “bila kutafuta ushauri kutoka katika kinywa changu.” #Tnn., “katika ngome ya Farao.”

SURA YA 29

a Ne 9:7
Mik 7:20

b Yoe 2:27

c Isa 45:11

d Isa 8:13
Ho 3:5

SURA YA 30

e Isa 1:2
Isa 63:10
Isa 65:2

f Isa 29:15

g Isa 31:1
Eze 29:6

h Hes 27:21
1Fa 22:7

i Yer 17:5

j Isa 19:11
Eze 30:14

Safu ya 2

a Isa 31:3
Yer 2:36

b Isa 31:1
Yer 37:7, 8

c Zb 87:4
Zb 89:10

d Isa 8:1
Yer 36:2

e Ro 15:4

f Kum 31:27
Isa 1:4
Yer 44:3

g Isa 59:3
Yer 9:3

h 2Nya 33:10
2Nya 36:15, 16
Ne 9:29
Yer 7:13

i 2Nya 16:10
2Nya 18:7
Yer 11:21
Yer 26:11

Na wajumbe wake wamefi-ka Hanesi.

5 Wote wataabishwa

Na watu ambao hawawezi kuwanufaisha,

Ambao hawawapi msaada wowote wala manufaa

yoyote,

Isipokuwa aibu na fedheha.”^a

6 Tangazo dhidi ya wanyama wa kusini:

Katika nchi ya taabu na hali ngumu,

Ya simba, simba anayenguruma,

Ya nyoka kipiri na nyoka wa moto arukaye,^{*}

Wanabeba mali zao juu ya migongo ya punda

Na mizigo yao juu ya ndu za ngamia.

Lakini vitu hivyo havitanufaisha watu.

7 Kwa maana msaada wa Misri haufai kitu.^b

Kwa hiyo nimemwita huyu: “Rahabu,^c anayeketi tuli.”

8 “Sasa nenda, iandike juu ya bamba mbele yao,

Na uiandike katika kitabu,^d

Ili itumike siku ya baadaye Kama ushahidi wa kudumu.^e

9 Kwa maana wao ni watu waasi,^f wana wadanga-nyifu,^g

Wana wasiotaka kusikia sheria^{*} ya Yehova.^h

10 Wanawaambia waonaji, ‘Msione,’

Na wale wanaopata maono, ‘Msituambia maono

ya kweli.’ⁱ

30:6 * Au “nyoka mwenye sumu anayeurukaru.” 30:9 * Au “mafundisho.”

Tuambieni mambo yanayotupendeza;* oneni maono ya udanganyifu.^a

- 11** Tokeni kwenye njia; ondo-keni kwenye kijia.

Acheni kumweka Mtakatifu wa Israeli mbele yetu.”^b

- 12** Kwa hiyo Mtakatifu wa Israeli anasema hivi: “Kwa kuwa mnalikataa neno hili^c

Nanyi mnatumaini ulaghai na udanganyifu Na mnayategemea mambo hayo,^d

- 13** Kwa hiyo uovu huu utakuwa kwenu kama ukuta uliobomoka,

Kama ukuta mrefu uliofura unaokaribia kuanguka.

Utaanguka ghafla, mara moja.

- 14** Utavunjwa kama mtungi mkubwa wa mfinyanzi,

Utapondwaponywa kabisa hivi kwamba hakuna kigae chochote kitakachobaki

Ili kitumiwe kukusanya moto jikoni

Au kuchota maji kutoka kwenye kidimbwi.”^{*}

- 15** Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, Mtakatifu wa Israeli, anasema hivi:

“Mkirudi kwangu na kupumzika, mtaokolewa;

Mtakuwa na nguvu mkien-ndeleva kuwa watulivu na kuwa na tumaini.”^e

Lakini hamkutaka.^f

- 16** Badala yake, mlisema:

30:10 *Tnn., “mambo laini.” **30:14**
*Au labda, “tangi la maji.”

SURA YA 30

a Yer 23:16, 17
Eze 13:7
Mik 2:11

b Amo 7:13, 16

c Amo 2:4, 5

d Yer 13:25
Mik 3:11

e 1Nya 5:20
2Nya 16:8
Isa 26:3

f Mt 23:37
Mdo 7:51

Safu ya 2

a Isa 31:1, 3

b Kum 28:49, 50
Yer 4:13
Omb 4:19
Hab 1:6, 8

c Law 26:36
Kum 32:30

d Eze 12:16

e Kut 34:6
Eze 36:9, 10

f Zb 102:13
Ro 9:15

g Zb 99:4
Yer 10:24

h Yer 17:7

i Ne 11:1
Isa 44:28
Isa 62:1
Yer 31:6
Zek 1:17

j Ne 12:27
Isa 61:3

k Yer 29:11, 12

l Law 26:26
Zb 80:5

m Ayu 36:22
Zb 32:8
Zb 71:17
Zb 119:102

n Zb 25:8, 9

o Kum 5:32
Yos 1:7, 8
Met 4:27

“Hapana, tutakimbia kwa farasi!”

Basi mtakimbia.

“Nasi tutapanda farasi wenye mbio!”^a

Kwa hiyo wale wanao-wafuata watakuwa na mbio.^b

- 17** Watu elfu moja watatetemeka wakitishwa na mtu mmoja;^c

Mtakapotishwa na watu watano mtakimbia

Mpaka mbaki kama mlingoti juu ya mlima,

Kama nguzo ya ishara juu ya kilima.^d

- 18** Lakini Yehova anangoja kwa subira* ili kuwao-nyesha kibali,^e

Naye atainuka ili kuwao-nyesha rehema.^f

Kwa maana Yehova ni Mungu wa haki.^g

Wenye furaha ni wote wanaoendelea kumtarajia.^h

- 19** Watu watakapokaa Sanyuni, Yerusalemu,ⁱ hutalia kamwe.^j Kwa hakika atakuonyesha kibali mara tu atakaposikia kilio chako cha kuomba msaada; atakujibu mara tu atakaposikia kilio chako.^k

- 20** Ingawa Yehova atawapa taabu kama mkate na ukandamizaji kama maji,^l Mfundishaji wako Mkuu hatajificha tena, nawe utamwona Mfundishaji wako Mkuu^m kwa macho yako mwenyewe. **21** Na masikio yako mwenyewe yatasikia neno nyuma yako likisema, “Hii ndiyo njia.” Tembeeni ndani yake,ⁿ ikiwa mtaenda upande wa kulia au mtaenda upande wa kushoto.^o

30:18 *Au “anaendelea kuwatarajia.”
*Au “wanaomgoja kwa hamu.”

22 Nanyi mtaitia unajisi fedha inayofunika sanamu zenu za kuchongwa na dhahabu inayofunika sanamu zenu za chuma.*^a Mtazitupa mbali kama kitambaa cha hedhi na kuziambia, "Potelea mbali!"^{#b} 23 Naye ataleta mvua kwa ajili ya mbegu mtakazopanda ardhini,^c na chakula* kitakachotoka ardhini kitakuwa kingi na chenye lishe.^{#d} Siku hiyo mifugo yenu italisha katika malisho makubwa.^e

24 Na ng'ombe na punda wanaolima mashamba wataku la chakula cha mifugo kilichokolezwa kwa mboga chungu, kilichopepetwa kwa setu na kwa uma. 25 Na juu ya kila mlima mrefu na juu ya kila kilima kirefu kutakuwa na vijito na mitaro ya maji,^f katika siku ya mauaji makubwa wakati ambapo minara itaanguka. 26 Na mwangaza wa mwezi mpevu utakuwa kama mwangaza wa jua; na mwangaza wa jua utaongezeka mara saba,^g kama mwangaza wa siku saba, katika siku ambayo Yehova atalifunga jeraha* la watu wake^h na kuponya kidonda kikubwa kilichosababishwa na pigo alilowaletea.ⁱ

27 Tazama! Jina la Yehova linakuja kutoka mbali sana, Likiwaka kwa hasira yake na kwa mawingu mazito. Midomo yake imejaa ghadhabu,

30:22 *Au "sanamu za kuyeyushwa." #Au labda, "na kuziita uchafu." 30:23 *Au "mkate." #Tnn., "mnono na wenye mafuta." 30:26 *Au "jeraha la kuvunijika."

SURA YA 30

a Kut 32:4
Kum 7:5, 25
Amu 17:3, 4

b Ho 14:8
Zek 13:2

c Zb 65:9
Zek 10:1

d Ho 2:21, 22

e Isa 65:10

f Isa 41:18
Isa 44:3

g Isa 60:20
Ufu 21:23
Ufu 22:5

h Omb 2:13

i Yer 33:6
Amo 9:11

Safu ya 2

a Isa 10:17
Nah 1:6
Sef 3:8

b 2Fa 19:28
Zb 32:9

c Kum 16:14
Zb 42:4
Yer 33:10, 11

d Kum 32:4
Isa 26:4

e Zb 29:3, 4

f Kut 15:16
Zb 98:1

g Nah 1:2

h Zb 18:13

i Amu 5:4

j Yos 10:11

k Isa 37:36

l Isa 10:12

m Kut 15:20
Amu 11:34

n Isa 10:24, 26

Na ulimi wake ni kama moto unaoteketeza.^a

28 Roho* yake ni kama mto unaofurika unaofika mpaka shingoni, Ili kuyatikisa mataifa katika chujio la maangamizi,[#]

Na mataifa yatakuwa na lijamu katika mataya yao^b ambayo inawapotosha.

29 Lakini wimbo wenu utakuwa kama wimbo unaoimbwa usiku Mnapojitayarisha* kwa ajili ya sherehe,^c

Na moyo wenu utashangilia kama mtu

Anayetembea na[#] filimbi Akielekea kwenye mlima wa Yehova, kwa Mwamba wa Israeli.^d

30 Yehova atafanya sauti yake kuu^e isikiwe

Naye ataonyesha mkono wake^f unaposhuka kwa hasira kali,^g

Ukiwa na mwali wa moto unaoteketeza,^h

Tufani ya mvua na dhoruba yenye ngurumoⁱ na mvua ya mawe.^j

31 Kwa maana kwa sababu ya sauti ya Yehova, Ashuru itashikwa na hofu;^k Ataipiga kwa fimbo.^l

32 Na kila pigo la fimbo yake ya adhabu Ambalo Yehova ataleta juu ya Ashuru Litaambatana na matari na vinubi^m Anapoutikisa mkono wake dhidi yao vitani.ⁿ

30:28 *Au "Pumzi." #Tnn., "chujio la ubatili." 30:29 *Au "mnapojitakasa." #Au "akisikia sauti ya."

33 Kwa maana tayari
Tofethi*^a yake ime-
tayarishwa;
Pia imetayarishwa kwa aji-
li ya mfalme.^b
Amefanya rundo la kuni
liwe na kina kirefu na
liwe pana,
Kwa wingi wa moto na
kuni.
Pumzi ya Yehova, kama
mto wa kiberiti,
Itaiwasha moto.

31 Ole wao wanaoshuka
kwenda Misri kuta-
futa msaada,^c
Wanaotegemea farasi,^d
Wanaotumaini magari ya
vita kwa sababu ni
mengi,
Na farasi wa vita* kwa
sababu wana nguvu.
Lakini hawamtegemei Mta-
katifu wa Israeli,
Na hawamtafuti Yehova.
2 Lakini yeye pia ana heki-
ma na ataleta msiba,
Naye hatayabatilisha
maneno yake.
Atainuka dhidi ya nyumba
ya watanda maovu
Na dhidi ya wale wanaowa-
saidia wakosaji.^e
3 Hata hivyo, Wamisri ni
wanadamu tu, wao si
Mungu;
Farasi wao ni nyama wala
si roho.^f
Yehova atakapounyoosha
mkono wake,
Yeyote atakayetoa msaada
atajikwaa
Na yeyote atakayesaidiwa
ataanguka;

30:33 *Hapa neno "Tofethi" linatumiwa kurejelea mahali pa mfano pa kuteke-tezea vitu, panafananisha maangamizi.
31:1 *Au "wapanda farasi."

SURA YA 30

a 2Fa 23:10
Yer 7:32b Isa 37:37, 38
Eze 32:22

SURA YA 31

c Isa 30:2

d Kum 17:15, 16

e Eze 29:6, 7

f Zb 33:17
Met 21:31

Safu ya 2

a Kum 32:11, 12
Zb 91:4b Isa 55:7
Yoe 2:12c 2Fa 19:35
2Nya 32:21
Isa 37:36

Wote wataangamia wakati
mmoja.

- 4** Kwa maana Yehova ame-
niambia hivi:
"Kama simba anavyo-
ngurume, mwanasimba
mwenye nguvu,* juu ya
mawindo yake,
Kundi lote la wachungaji
linapokusanywa kupiga-
na naye,
Naye haogopi sauti yao
Au kutishwa na kelele zao,
Ndivyo Yehova wa majeshi
atakavyoshuka ili kupi-
gana vita
Juu ya Mlima Sayuni na
juu ya kilima chake.
5 Kama ndege wanaoshuka
kwa ghafla, ndivyo Yeho-
va wa majeshi
atakavyolilinda Yerusa-
lemu.^a
Atalilinda na kuliokoa.
Atalihifadhi na kuliokoa."
6 "Rudini kwa Yule amba-
ye mmemwasi bila aibu, enyi
watu wa Israeli.^b **7** Kwa ma-
na siku hiyo kila mmoja atai-
kataa miungu yake ya ubatili
ya fedha na miungu yake ya
dhahabu ambayo haina tha-
mani, ambayo mikono yenu
wenyewe ilitenda dhambi kwa
kuitengeneza.
8 Na Mwashuru atauawa
kwa upanga, lakini si wa
mwanadamu;^c
Na upanga, usio wa
mwanadamu, utamwa-
ngamiza.
Atakimbia kwa sababu ya
upanga,
Na wanaume wake vijana
watalazimishwa kufanya
kazi za kulazimishwa.

31:4 *Au "mwanasimba mwenye ma-nyoya marefu shingoni."

- 9 Jabali lake litapitilia mbali kwa sababu ya woga mwingi,
Na wakuu wake wataogopa kwa sababu ya nguzo ya ishara,” asema Yehova, Ambaye nuru yake iko*
Sayuni na ambaye tanuru lake liko Yerusalemu.
- 32** Tazama! Mfalme^a atatawala kwa uadilifu,^b
Na wakuu watatawala kwa haki.
- 2 Na kila mmoja atakuwa kama mahali pa kujificha* kutokana na upepo,
Na mahali pa kujisitiri[#] kutokana na dhoruba ya mvua,
Kama vijito vya maji katika nchi isiyo na maji,^c
Kama kivuli cha jabali kubwa katika nchi iliyo-kauka.
- 3 Kisha macho ya wale wanaoona hayatafungwa tena,
Na masikio ya wale wanaosikia yatasikiliza.
- 4 Moyo wa wale wanaofanya mambo bila kufikiri utatafakari ujuzi,
Na ulimi wa wenye kigugumizi utazungumza kwa ufasaha na waziwazi.^d
- 5 Mtu mpumbavu hataitwa tena mkarimu,
Na mtu asiye na msimamo hataitwa mheshimiwa;
- 6 Kwa maana mtu mpumbavu atazungumza upumbavu,
Na moyo wake utatunga mambo yanayodhuru,^e

31:9 *Au “moto wake uko.” 32:2 *Au “kibanda cha kujificha.” #Au “mahali pa kukimbilia.”

SURA YA 32

a Mwa 49:10
Zb 2:6
Lu 1:32, 33
Yoh 1:49

b Zb 45:6
Zb 72:1
Isa 9:7
Isa 11:4, 5
Yer 23:5
Zek 9:9
Ebr 1:9
Ufu 19:11

c Isa 35:6

d Isa 35:6

e Mik 2:1

Safu ya 2

a Yer 5:26
Mik 7:3

b 1Fa 21:9, 10

c Isa 3:16

d Omb 2:12
Sef 1:13

e Isa 3:24

Ili kuendeleza uasi imani*
na kusema mambo mapotovu dhidi ya Yehova,
Kusababisha mwenye njaa akae njaa

Na kumnyima mwenye kiu maji ya kunywa.

- 7 Mipango ya mtu asiye na msimamo ni mibaya;^a

Anaendeleza mwenendo wa aibu

Ili kumwagamiza kwa uwongo mtu anayeteseka,^b

Hata maskini anaposema jambo lililo sawa.

- 8 Lakini mtu mkarimu anania ya ukarimu,

Naye huendelea kutenda matendo ya ukarimu.*

- 9 “Enyi wanawake mnaopuza mambo, simameni msikilize sauti yangu!

Enyi mabinti msiojali,^c sikilizeni ninachosema!

- 10 Katika muda unaozidi mwaka mmoja hivi, ninyi msiojali mtatetemeka,

Kwa sababu hakuna matunda yatakayokuwa yamekusanywa mavuno ya zabibu yatakapokwisha.^d

- 11 Tetemekeni, ninyi wanawake mnaopuza mambo!

Tetemekeni, ninyi msiojali! Vueni nguo mbaki uchi, Na mvae nguo za magunia viunoni.^e

- 12 Pigeni vifua vyenu kwa kuomboleza

Kwa sababu ya mashamba yanayotamanika na mzabibu unaozaa matunda mengi.

32:6 *Au “kutenda kwa kutomwogopa Mungu.” 32:8 *Au “matendo mema.”

- 13** Kwa maana ardhi ya watu wangu itafunikwa kwa miiba na michongoma; Itazifunika nyumba zote zenye furaha, Naam, jiji la shangwe.^a
- 14** Kwa maana mnara wenye ngome umeachwa; Jiji lenye kelele limeachwa.^b Ofeli^c na mnara wa mlinzi vimebaki ukiwa daima, Mahali panapopendwa na punda wa mwituni, Malisho ya mifugo,^d
- 15** Mpaka roho itakapomiminda juu yetu kutoka juu,^e Na nyika iwe shamba la matunda, Na shamba la matunda lio-nwe kuwa msitu.^f
- 16** Kisha haki itakaa nyikani, Na uadilifu utakaa katika shamba la matunda.^g
- 17** Matokeo ya uadilifu wa kweli yatakuwa amani,^h Na mazao ya uadilifu wa kweli yatakuwa utulivu wa kudumu na usalama wa kudumu.ⁱ
- 18** Watu wangu watakaa katika makao ya kudumu yenye amani, Katika makao salama na mahali pa kupumzika penye utulivu.^j
- 19** Lakini mvua ya mawe itauangusha chini msitu, Na jiji litabomolewa kabisa.
- 20** Wenye furaha ni ninyi mnaopanda mbegu kando ya maji yote, Mnaowatoa nje* ng'ombe dume na punda.^k

32:20 *Au "Mnaowafungua."

SURA YA 32

a Isa 22:2
Omb 2:15

b 2Fa 25:9, 10

c 2Nya 27:1, 3
Ne 3:26

d Isa 27:10

e Isa 44:3

f Isa 29:17
Isa 35:1, 2g Isa 42:1, 4
Isa 60:21h Zb 119:165
Isa 55:12i Eze 37:26
Mik 4:3, 4j Isa 60:18
Isa 65:22
Yer 23:6
Eze 34:25
Ho 2:18

k Isa 30:23, 24

Safu ya 2

SURA YA 33

a 2Fa 18:13
Isa 10:5b Isa 10:12
Nah 3:7

c Zb 123:2

d Zb 44:3
Isa 52:10e Zb 46:1
Nah 1:7f Zb 46:6
Zb 68:1
Isa 17:13

g Zb 27:1

h Met 19:23

33 Ole wako wewe, mwan-gamizaji ambaye hujaangamizwa,^a

Ewe msaliti ambaye huja-salitiwa!

Utakapomaliza kuanga-miza, utaangamizwa.^b

Utakapomaliza kusaliti, utasalitiwa.

2 Ee Yehova, tuonyeshe kibali.^c

Tunakutumaini wewe.

Uwe mkono wetu*^d kila asubuhi,

Naam, wokovu wetu waka-ti wa taabu.^e

3 Watu wanakimbia kwa sa-babu ya sauti ya ghasia.

Unapoinuka, mataifa yanatawanyika.^f

4 Kama nzige wanaokula sana wanavyokusanyika,

ndivyo nyara zako zita-kavyokusanywa;

Watu watazikimbilia kama makundi ya nzige.

5 Yehova atakwezwa,

Kwa maana anakaa katika vilele vilivyo juu.

Ataijaza Sayuni haki na uadilifu.

6 Yeye ndiye tegeme imara la nyakati zako;

Wingi wa wokovu,^g hekima, ujuzi, na

kumwogopa Yehova^h

—Hiyo ndiyo hazina yake.

7 Tazama! Mashujaa wao wanalia kwa sauti barabarani;

Wajumbe wa amani wana-lia kwa uchungu.

8 Barabara kuu zimebaki tupu;

Hakuna mtu anayesafiri kwenye vijia.

33:2 *Au "nguvu zetu."

- Amelivunja* agano;
Ameyakataa majiji;
Hamheshimu mwanadamu
anayeweza kufa.^a
- 9** Nchi inaomboleza* na kunyauka kabisa.
Lebanoni imeaibika;^b
imeoza.
Sharoni imekuwa kama jangwa,
Na Bashani na Karmeli zinapukutisha majani yake.^c
- 10** "Sasa nitainuka," asema Yehova,
"Sasa nitajikweza mwenyewe;^d
Sasa nitajitukuza mwenyewe.
- 11** Mnachukua mimba ya majani yaliyokauka na kuzaa majani makavu.
Roho yenu wenyewe itawateketeza kama moto.^e
- 12** Na watu watakuwa kama chokaa iliyoteketea.
Watawashwa moto kama miiba iliyokatwa.^f
- 13** Ninyi mlio mbali sana, sikieni jambo nitakalofanya!
Nanyi mlio karibu, tambueni uwezo wangu!
- 14** Watenda dhambi walio Sayuni wanaogopa;^g
Waasi imani wanatetemeka:
'Ni nani kati yetu anayeweza kuishi mahali palipo na moto unaoteketeza?^h
Ni nani kati yetu anayeweza kuishi na miale isiyoweza kuzimwa?'
- 15** Yule anayetembea katika uadilifu wa daima,ⁱ

33:8 *Yaani, adui. 33:9 *Au labda, "inakauka."

SURA YA 33

a 2Fa 18:19, 20

b Isa 37:24

c Nah 1:4

d Zb 46:10

e Isa 5:24

f Isa 9:18

g Kum 28:66, 67

h Kum 32:22
Nah 1:6
Ebr 12:29

i Eze 18:17

Safu ya 2

a 1Nya 29:17

b Kut 23:8
Kum 16:19

c 1Fa 19:5, 6
Zb 34:9, 10
Isa 65:13

d 2Fa 15:19

e Kum 28:49, 50
Isa 28:11
Yer 5:15

f Kum 12:5, 6

- Anayesema mambo manyoofu,^a
Anayekataa faida isiyo ya haki, ya ulaghai,
Ambaye mikono yake inakataa rushwa badala ya kuichukua kwa nguvu,^b
Anayeziba sikio lake ili lisisikilize mazungumzo ya umwagaji wa damu,
Na anayefunga macho yake ili yasione maovu
- 16** –Atakaa katika vilele;
Kimbilio lake salama* lita-kuwa katika ngome zilizo kwenye miamba,
Atapewa mkate wake,
Naye maji yake hayataisha kamwe."^c
- 17** Macho yako yatamwona mfalme katika fahari yake;
Yataona nchi iliyo mbali sana.
- 18** Moyoni mwako utakumbuka* jambo linaloogopesha:
"Yuko wapi mwandishi? Yuko wapi yule aliyepima ushuru?^d
Yuko wapi yule aliyehesabu minara?"
- 19** Hutawaona tena watu wenyewe dharau,
Watu ambao lugha yao ni ngumu sana kueleweka,*
Ambao huwezi kuelewa ulimi wao wenye kigugumizi.^e
- 20** Tazama Sayuni, jiji la she-rehe zetu!^f
Macho yako yataona Yerusalemu kama makao matulivu,

33:16 *Au "kilele salama." 33:18 *Au "utatafakari." 33:19 *Tnn., "ina kina kirefu isiweze kueleweka."

Hema ambalo halitaondo-
lewa.^a

Vigingi vyake vya mahema
havitang'olewa kamwe,
Na hakuna kamba yake
yoyote itakayokatwa.

21 Lakini huko, yule Aliye
Mkuu, Yehova,
Atakuwa kwetu eneo la
mito, la mifereji mipana,
Ambako hakuna kundi
la merikebu litakaloenda
huko

Na hakuna meli za kifahari
zitikazopita huko.

22 Kwa maana Yehova ni
Mwamuzi wetu,^b
Yehova ni Mpaji-sheria
wetu,^c
Yehova ni Mfalme wetu;^d
Yeye Ndiye atakayetu-
okoa.^e

23 Kamba zako zitalegea na
kuning'inia;
Haziwezi kushika mlingoti
usimame imara wala ku-
tandaza tanga.
Wakati huo nyara nyingi
zitagawanywa;
Hata mtu mlemavu ata-
chukua nyara nyingi.^f

24 Na hakuna mkaaji* ata-
kayesema: "Mimi ni
mgonjwa."^g
Watu wanaokaa katika
nchi watasamehewa
dhambi yao.^h

34 Njoooni karibu ili msikie,
enyi mataifa,
Na msikilize, enyi watu.
Dunia na vyote vinavyoija-
za na visikilize,
Nchi na mazao yake yote.

2 Kwa maana hasira ya Ye-
hova inawaka dhidi ya
mataifa yote,ⁱ

SURA YA 33

a Zb 125:1

b Mwa 18:25
Zb 50:6
Zb 98:9

c Law 26:3
Yak 4:12

d Zb 44:4
Zb 97:1
Ufu 11:15, 17

e Isa 12:2
Sef 3:17

f Isa 33:4

g Kum 7:15
Ufu 21:4
Ufu 22:1, 2

h Yer 50:20
Mik 7:18, 19

SURA YA 34

i Yer 25:15
Yoe 3:12
Sef 3:8
Zek 14:3

Safu ya 2

a Isa 30:27
Nah 1:2

b Ufu 19:11, 15

c Yer 25:33

d Eze 39:4

e Kum 32:41

f Zb 137:7
Yer 49:7, 22

g Law 3:16

h Isa 63:1-3
Oba 8, 9

Na ghadhabu yake dhidi ya
jeshi lao lote.^a

Atawaangamiza;
Atawachinja.^b

3 Watu wao waliouawa wata-
tupwa nje,
Na uvundo wa maiti zao
utapaa;^c

Milima itayeyuka kwa sa-
babu ya* damu yao.^d

4 Jeshi lote la mbinguni li-
taoza kabisa,
Na mbingu zitakunjwa
kama kitabu cha kuku-
njwa.

Jeshi lake lote litanyauka
kabisa,

Kama jani lililonyauka li-
navyoanguka kutoka
kwenye mzabibu

Na tini iliyonyauka kutoka
kwenye mtini.

5 "Kwa maana upanga
wangu utaloweshwa mbi-
nguni.^e

Utashuka juu ya Edomu
katika hukumu,^f

Juu ya watu ambao nilia-
mua kuwaangamiza.

6 Yehova ana upanga; uta-
funikwa kwa damu.

Utafunikwa kwa mafuta,^g
Kwa damu ya wanakondoo
dume na mbuzi,

Kwa mafuta ya figo za ko-
ndoo dume.

Kwa maana Yehova ana
dhabihu kule Bosra,
Machinjo makubwa katika
nchi ya Edomu.^h

7 Fahali mwitu watashuka
pamoja nao,
Ng'ombe dume wachanga
watashuka pamoja na
wenye nguvu.

Nchi yao itajaa damu,

- Na mavumbi yao yatalowa mafuta.”
- 8** Kwa maana Yehova ana siku ya kisasi,^a
Mwaka wa malipo ya kesi dhidi ya Sayuni.^b
- 9** Vijito vyake* vitabadilishwa kuwa lami,
Na mavumbi yake kuwa kiberiti,
Na nchi yake itakuwa kama lami inayowaka.
- 10** Haitazimwa usiku wala mchana;
Moshi wake utaendelea kupaa milele.
Itabaki ukiwa kizazi baada ya kizazi;
Hakuna yeyote atakayepita katikati yake milele na milele.^c
- 11** Mwari na nungunungu wataimiliki,
Na bundi wenye masikio marefu na kunguru watakaa ndani yake.
Atanyoosha juu yake kamba ya kupimia ya utupu
Na timazi* ya ukiwa.
- 12** Hakuna yeyote kati ya watu wake mashuhuri atakayepewa ufalme,
Na wakuu wake wote watakuwa si kitu.
- 13** Miiba itaota katika minara yake yenye ngome,
Upupu na magugu yenye miiba katika ngome yake.
Nchi hiyo itakuwa makao ya mwamwitu,^d
Boma la mbuni.
- 14** Viumbe wa jangwani watakutana na wanyama wanaopiga mayowe,

34:9 *Inaonekana vinarejelea Bosra, jiji kuu la Edomu. 34:11 *Tnn., “mawe.”

SURA YA 34

a Kum 32:41
Zb 94:1

b Isa 35:4

c Mal 1:4

d Mal 1:3

Safu ya 2

SURA YA 35

a Isa 29:17
Isa 32:14, 15

b Isa 4:2
Isa 27:6
Isa 35:6
Isa 51:3
Eze 36:35

c Ho 14:5, 6

d Isa 60:13

e Yer 50:19

f Isa 65:10

Na mbuzi wa mwituni* atamwita mwenzake.

Naam, huko babewatoto atakaa na kupata mahali pa kupumzika.

- 15** Nyoka-pili atatengeneza kiota chake huko na kutaga mayai,
Naye atayaangua na kuyakusanya katika kivuli chake.
Naam, vipanga watakusanyika huko, kila mmoja na mwenzake.
- 16** Tafutoni katika kitabu cha Yehova na mkisome kwa sauti:

Hakuna hata mmoja wao atakayekosekana;

Hakuna hata mmoja wao atakayekosa mwenzake,
Kwa maana kinywa cha Yehova ndicho kimeamuru,
Na roho yake ndiyo imewakusanya pamoja.

- 17** Yeye Ndiye amewapigia kura,
Na mkono wake mwenyewe umewapimia mahali walipogawiwa.*
Wataimiliki daima;
Watakaa ndani yake kwa vizazi vyote.

35 Nyika na nchi iliyokauka zitafurahi,^a

Na jangwa tambarare litashangilia na kuchanua maua kama zafarani.^b

- 2** Hakika itachanua maua;^c
Itashangilia na kupiga vigegelele vya shangwe.
Itapewa utukufu wa Lebanoni,^d
Fahari ya Karmeli^e na ya Sharoni.^f

34:14 *Au labda, “Na roho waovu walio kama mbuzi.” 34:17 *Tnn., “umewagawia kwa kamba ya kupimia.”

Watauona utukufu wa Yehova, fahari ya Mungu wetu.

3 Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu,

Na nyaimarishe magoti yanayotetemeka.^a

4 Waambieni wale wanaohangaika moyoni:
"Iweni na nguvu. Msio-gope.

Tazameni! Mungu wenu atakuja na kisasi, Mungu atakuja na malipo.^b Atakuja na kuwaokoa ninyi."^c

5 Wakati huo macho ya vipofu yatafunguliwa,^d Na masikio ya viziwi yatazibuliwa.^e

6 Wakati huo kilema ataruka kama paa,^f Na ulimi wa bubu utapiga vigelegele vya shangwe.^g Kwa maana maji yatabubujika nyikani, Na vijito katika jangwa tamarare.

7 Na ardhi iliyokaushwa na joto itakuwa kama dimbwi lenye matete, Na ardhi yenye kiu itakuwa kama mabubujiko ya maji.^h

Katika makao ambamo mbwamwitu walipumzika,ⁱ

Kutakuwa na majani mabichi na matete na mafunjo.

8 Na huko kutakuwa na barabara kuu,^j

Naam, njia inayoitwa Njia ya Utakatifu.

Mtu asiye safi hatasafiri kwenye njia hiyo.^k

Imetengwa kwa ajili ya yule anayetembea katika njia hiyo;

SURA YA 35

a Ebr 12:12

b Yer 51:56

c Isa 25:9
Sef 3:16, 17

d Zb 146:8
Isa 42:16
Mt 9:28-30

e Isa 29:18
Yer 6:10
Mk 7:32-35
Lu 7:22

f Mt 11:5
Mdo 8:7
Mdo 14:8-10

g Mt 15:30

h Isa 44:3

i Yer 9:11

j Ebr 1:3
Isa 11:16
Isa 49:11
Isa 62:10
Yer 31:21

k Isa 52:1

Safu ya 2

a Isa 11:6, 7
Isa 65:25
Eze 34:25
Ho 2:18

b Zb 107:2, 3
Isa 62:12

c Kum 30:4

d Isa 51:11
Yer 31:11, 12

e Yer 33:10, 11

f Isa 30:19
Isa 65:19

SURA YA 36

g Isa 10:5

h 2Fa 18:13
2Nya 32:1
Isa 8:7, 8
Isa 10:28-32
Isa 33:8

i 2Nya 32:9

j 2Fa 19:8

k Isa 7:3

l 2Fa 18:17, 18

m Isa 22:20, 21

n 2Fa 19:2

Hakuna mtu yeyote mpu-mbavu atakayepotea na kuingia katika njia hiyo.

9 Hakuna simba atakayekuwawako,

Na hakuna wanyama hatari wa mwituni watakaokuja kwenye njia hiyo.

Hawatapatikana huko;^a

Wale waliokombolewa tu ndio watakaotembea katika njia hiyo.^b

10 Wale waliokombolewa na Yehova watarudi^c na kuja Sayuni kwa kilio cha shangwe.^d

Shangwe isiyo na kikomo itakuwa taji la vichwa vyao.^e

Watapata shangwe na furaha,

Na huzuni na kilio cha uchungu vitatoweka.^f

36 Katika mwaka wa 14 wa utawala wa Mfalme Hezekia, Senakeribu mfalme wa Ashuru^g alipanda kuja kuya-shambulia majiji yote yenye ngome ya Yuda na kuyateka.^h

2 Kisha mfalme wa Ashuru akamtuma Rabshakeⁱ pamoja na jeshi kubwa kutoka Lakhish^j kwenda kwa Mfalme Hezekia kule Yerusalemu. Wakajipanga karibu na mfereji wa kidimbwi cha juu,^k kwenye barabara kuu ya uwanja wa mfuaji wa nguo.^l **3** Ndi-po Eliakimu^m mwana wa Hil-
kia, aliyekuwa msimamizi wa nyumba, * Shebnaⁿ aliyekuwa mwandishi, na Yoa mwana wa Asafu aliyefanya kazi ya kuweka kumbukumbu wakaenda nje kukutana naye.

36:2 *Au "msimamizi mkuu wa vinywaji vya mfalme." **36:3** *Au "jumba la mfalme."

4 Basi Rabshake akawambia: "Tafadhali, mwambieni hivi Hezekia: 'Mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru, anauliza, "Ujasiri wako unategemea msingi gani?"^a 5 Unasema, "Nina mbinu na nguvu za kupigana vita,' lakini hayo ni maneno matupu. Unamtumaini nani, hivi kwamba unathubutu kuniasi?"^b 6 Tazama! Unautumaini msaada wa utete huu uliopondeka, Misri, ambao mtu yeyote akiuegemea utamchoma kiganja na kukitoboa. Hivyo ndivyo Farao mfalme wa Misri alivyo kwa wote wanaomtumaini.^c 7 Nawe ukiniambia, 'Tunamtumaini Yehova Mungu wetu,' je, si yeye ndiye ambaye mahali pake pa juu na madhabahu zake zimeondolewa na Hezekia,^d huku akiwambia watu wa Yuda na Yerusalemu, 'Mnapaswa kuinama mbele ya madhabahu hii?'"^e 8 Basi sasa, tafadhali, fanya mkataba huu pamoja na bwana wangu mfalme wa Ashuru:^f nitakupa farasi 2,000 ikiwa unaweza kupata wapanda farasi wa kutosha idadi hiyo. 9 Basi, unawezaje kumzuia hata gavana mmoja aliye mdogo zaidi kati ya watumishi wa bwana wangu, huku ukiitumaini nchi ya Misri ili upate magari ya vita na wapanda farasi? 10 Sasa je, nimepanda kuja kuishambulia nchi hii ili kuiharibu bila kupewa idhini na Yehova? Yehova mwenyewe aliniambia, 'Panda uende kuishambulia nchi hii na kuiharibu.'"

11 Ndipo Eliakimu na Shebana^g na Yoa wakamwambia Rabshake:^h "Tafadhali, zungumza nasi watumishi wako kwa

SURA YA 36

a 2Fa 18:19-25
2Fa 19:10

b 2Fa 18:1, 7

c 2Fa 17:4
Isa 30:2, 7
Yer 37:7d 2Fa 18:1, 4
2Nya 31:1e Kum 12:11
2Nya 7:12
2Nya 32:12

f 2Fa 18:13

g Isa 22:15

h 2Fa 18:17

Safu ya 2

a Ezz 4:7
Da 2:4

b 2Fa 18:26, 27

c 2Nya 32:18

d 2Fa 18:28-35

e 2Nya 32:11, 15
Da 3:15

f 2Fa 19:22

g 2Fa 17:6
2Fa 17:22, 23

lugha ya Kiaramu*^a kwa maana tunaweza kuelewa; usizungumze nasi kwa lugha ya Wayahudi huku watu walio ukutani wakisikia."^b 12 Lakini Rabshake akasema: "Je, bwana wangu amenituma niwambia ninyi na bwana wenu tu maneno haya? Je, sipaswi kuwaambia pia wanaume wanaoketi ukutani, wale watakaokula kinyesi chao wenyewe na kunywa mkojo wao wenyewe pamoja nanyi?"

13 Kisha Rabshake akasimama na kusema hivi kwa sauti kubwa kwa lugha ya Wayahudi:^c "Sikieni neno la mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru."^d

14 Mfalme anasema hivi, 'Msikubali Hezekia awadanganaye, kwa maana hawezi kuwaokoa.^e 15 Na msikubali Hezekia awafanye mumtumaini Yehova^f mkisema: "Kwa hakika Yehova atatuokoa, na jiji hili halitatiwa mikononi mwa mfalme wa Ashuru." 16 Msimkilize Hezekia, kwa maana mfalme wa Ashuru anasema hivi: "Fanyeni amani pamoja nami na mjisalimishe,* na kila mmoja wenu atakula matunda ya mzabibu wake mwenyewe na matunda ya mtini wake mwenyewe na kunywa maji kutoka katika tangi lake mwenyewe, 17 mpaka nitakapokuja na kuwapeleka katika nchi iliyo kama nchi yenu wenyewe,^g nchi yenye nafaka na divai mpya, nchi yenye mikate na mashamba ya mizabibu. 18 Msikubali Hezekia awapotoshe akisema, 'Yehova atatuokoa.' Je, kuna mungu yeyote kati ya miungu ya ma-

36:11 *Au "Kisiria." 36:16 *Tnn., "Fanyeni baraka pamoja nami na mtoke nje na kuja kwangu."

taifa ambaye amewahi kui-
koa nchi yake kutoka miko-
noni mwa mfalme wa Ashu-
ru?^a **19** Iko wapi miungu ya
Hamathi na Arpadi?^b Iko wapi
miungu ya Sefarvaimu?^c Na je,
imeokoa Samaria kutoka mi-
kononi mwangu?^d **20** Ni mu-
ngu yupi kati ya miungu yote
ya nchi hizi ambaye ameokoa
nchi yake kutoka mikononi
mwangu, hivi kwamba Yehova
aokoe Yerusalemu kutoka mi-
kononi mwangu?^e

21 Lakini walikaa kimya,
hawakumjibu neno lolote, kwa
maana mfalme aliwaagiza hivi:
“Msimjibu.”^f **22** Lakini Elia-
kimu mwana wa Hilkia, aliye-
kuwa msimamizi wa nyumba,*
Shebna^g aliye kuwa mwandishi,
na Yoa mwana wa Asa-
fu aliye kuwa akifanya kazi ya
kuweka kumbukumbu waka-
ja kwa Hezekia mavazi yao ya-
kiwa yameraruliwa, wakamwa-
mbia maneno ya Rabshake.

37 Mara tu Mfalme Heze-
kia aliposikia hilo, aka-
yararua mavazi yake na ku-
vaa nguo za magunia na
kuingia katika nyumba ya
Yehova.^h **2** Kisha akamtuma
Eliakimu, aliye kuwa msima-
mizi wa nyumba,* Shebna ali-
ye kuwa mwandishi, na wazee
miongoni mwa makuhani, wa-
kiwa wamevaa nguo za ma-
gunia, waende kwa nabii Isa-
ya,ⁱ mwana wa Amози. **3** Wa-
kamwambia: “Hezekia anase-
ma hivi: ‘Leo ni siku ya taabu,
ya kemeo,* na ya aibu; kwa
maana watoto wako tayari ku-
zaliwa’ lakini hakuna nguvu
za kuwazaa.’” **4** Huenda Ye-
hova Mungu wako atayasikia

36:22; 37:2 *Au “jumba la mfalme.”
37:3 *Au “matusi.” #Tnn., “wamefika
kwenye mlango wa tumbo la uzazi.”

SURA YA 36

a 2Fa 19:11, 12
2Nya 32:14
Isa 37:11, 12

b Yer 49:23

c 2Fa 17:24

d 2Fa 17:6
2Fa 17:22, 23
Isa 10:11

e 2Fa 19:17, 18
2Nya 32:15
Isa 37:23

f 2Fa 18:36, 37
Met 9:7

g Isa 22:15

SURA YA 37

h 2Fa 19:1-4

i 2Nya 26:22
Isa 1:1

j Isa 26:17, 18

Safu ya 2

a 1Sa 17:45
2Fa 18:28, 35

b 2Nya 32:20
Zb 50:15
Yoe 2:17

c 2Fa 17:18

d 2Fa 19:5-7

e Kum 20:1

f 2Fa 18:17

g Met 21:1

h 2Nya 32:21
Isa 37:37, 38

i Yos 10:29, 30
2Fa 8:22
2Fa 19:8-13

j 2Fa 18:17

k 2Nya 32:15

l 2Fa 17:5, 6
2Nya 32:13
Isa 10:11

maneno ya Rabshake, aliyetu-
mwa na bwana wake mfalme
wa Ashuru ili amdhihaki Mu-
ngu aliye hai,^a naye atamfanya
awajibike kwa sababu ya ma-
neno ambayo Yehova Mungu
wako amesikia. Basi toa sala^b
kwa niaba ya watu waliobaki
ambao wameokoka.”^c

5 Kwa hiyo watumishi wa
Mfalme Hezekia wakaenda
kwa Isaya,^d **6** naye Isaya
akawaambia: “Mwambieni hivi
bwana wenu, ‘Yehova anase-
ma hivi: “Usiogope^e kwa saba-
bu ya maneno uliyosikia, ma-
neno ambayo watumishi wa
mfalme wa Ashuru^f waliyase-
ma na kunikufuru. **7** Sasa ni-
natia wazo fulani akilini mwa-
ke,* naye atasikia habari na
kurudi katika nchi yake mwe-
nyewe;^g nami nitamua kwa
upanga katika nchi yake mwe-
nyewe.””^h

8 Baada ya Rabshake kusi-
kia kwamba mfalme wa Ashu-
ru ameondoka Lakishi, aliru-
di na kumkuta akipigana vita
na Libna.ⁱ **9** Ndipo mfalme
akasikia maneno haya yakise-
mwa kumhusu Tirhaka mfal-
me wa Ethiopia: “Amekuja
ili kupigana nawe.” Aliposi-
kia hivyo, akawatuma tena
wajumbe kwa Hezekia,^j aki-
sema: **10** “Mwambieni hivi
Mfalme Hezekia wa Yuda,
‘Usikubali Mungu wako una-
yemtumaini akudanganye aki-
sema: “Yerusalemu halitati-
wa mikononi mwa mfalme wa
Ashuru.”^k **11** Tazama! Ume-
sikia mambo ambayo wafal-
me wa Ashuru walizitendea
nchi zote kwa kuziangamiza.^l
Je, ni wewe peke yako uta-
kayeokolewa? **12** Je, miungu

37:7 *Tnn., “ninatia roho fulani ndani
yake.”

ya mataifa yaliyoangamizwa na mababu zangu iliyaokoa mataifa hayo?^a Gozani, Harani,^b Resefu, na watu wa Ede-ni waliokuwa Tel-asari wako wapi? **13** Yuko wapi mfalme wa Hamathi, mfalme wa Arpa-di, na mfalme wa majiji ya Se-farvaimu,^c na wa Hena, na wa Iva?”

14 Hezekia akachukua barua hizo kutoka mikononi mwa wajumbe na kuzisoma. Kisha Hezekia akapanda kwenda kati-tika nyumba ya Yehova, akazitandaza* mbele za Yehova.^d

15 Hezekia akaanza kusali kwa Yehova^e akisema: **16** “Ee Yehova wa majeshi,^f Mungu wa Israeli, unayeketi kwenye kiti cha ufalme juu ya* ma-kerubi, wewe peke yako ndi-ye Mungu wa kweli wa falme zote za dunia. Uliumba mbin-gu na dunia. **17** Tega sikio lako, Ee Yehova, usikie!^g Fun-gua macho yako, Ee Yeho-va, uone!^h Sikia maneno yote ambayo Senakeribu amese-ma ili kukudhihaki wewe Mun-gu uliye hai.ⁱ **18** Ee Yeho-va, ni kweli kwamba wafalme wa Ashuru wameharibu nchi zote,^j na pia nchi yao. **19** Nao wameitupa miungu yao moto-ni,^k kwa sababu haikuwa miun-gu bali kazi ya mikono ya wa-nadamu,^l miti na mawe. Ndiyo sababu waliweza kuiangamiza. **20** Lakini sasa, Ee Yehova Mun-gu wetu, tuokoe kutoka mi-kononi mwake, ili falme zote duniani zijue kwamba wewe peke yako ndiye Mungu, Ee Yeh-ova.”^m

21 Kisha Isaya mwana wa Amози akatuma ujumbe huu kwa Hezekia: “Yehova Mu-

37:14 *Tnn., “akaitandaza.” 37:16 *Au labda, “katikati ya.”

SURA YA 37

a Isa 36:19

b Mwa 11:31

c 2Fa 17:24
Isa 36:19

d 2Fa 19:14-19

e 1Fa 8:30
2Nya 6:20
2Nya 20:9
Da 9:3f Zb 46:7
Isa 8:13g 2Nya 6:40
Zb 65:2h 2Nya 16:9
1Pe 3:12

i Isa 37:4

j 2Fa 15:29
2Fa 16:8, 9
1Nya 5:26

k Isa 10:11

l Isa 40:19
Isa 41:7
Yer 10:3
Ho 8:6
Mdo 17:29m Kum 32:31, 39
Zb 83:18
Zb 96:5

Safu ya 2

a 2Fa 19:20, 21

b 2Fa 19:4, 16

c 2Fa 18:30, 35
Isa 10:12, 13d Kut 15:11
2Fa 19:22-24
Isa 10:20
Eze 39:7

e 2Nya 32:17

f Isa 10:10, 11

g Zb 33:11
Isa 46:10

h Isa 55:10, 11

ngu wa Israeli anasema, ‘Kwa sababu ulisali kwangu kuhusu Mfalme Senakeribu wa Ashuru.’^a **22** Hili ndilo neno ambalo Yehova amesema dhidi yake:

“Binti bikira wa Sayuni anakudharau, anakudhihaki.

Binti ya Yerusalemu anakutikisia kichwa.

23 Umemdhihaki^b na kumkufuru nani?

Umepaza sauti yako dhidi ya nani^c

Na kuinua macho yako yenye kiburi?

Ni dhidi ya Mtakatifu wa Israeli!^d

24 Kupitia watumishi wako umemdhihaki Yehova^e ukisema,

‘Kwa wingi wa magari yangu ya vita

Nitapanda vilele vya milima,^f

Sehemu za mbali sana za Lebanoni.

Nitakata mierezi yake mirefu sana, miberoshi yake iliyo bora.

Nitaingia mahali pake pali-po juu zaidi, misitu yake yenye miti mingi sana.

25 Nitachimba visima na kuniywa maji;

Nitavikausha vijito vya* Misri kwa nyayo za mi-guu yangu.’

26 Je, hujasikia? Tangu zamani za kale lilia-muliwa.*

Tangu siku zilizopita nime-litayarisha.^{#g}

Sasa nitalitimiza.^h

37:25 *Au “Nitaikausha mifereji ya Nile ya.” 37:26 *Tnn., “lilifanywa.” #Au “nimelitengeneza.”

Utayabadili majiji yenye ngome yawe marundo ya magofu yenye ukiwa.^a

27 Wakaaji wake hawatakuwa na uwezo;

Wataogopeshwa na kuaibishwa.

Watakuwa kama mimea ya shambani na nyasi mbichi,

Kama nyasi zilizo kwenye paa zinazokaushwa na upepo wa mashariki.

28 Lakini ninajua vizuri unapoketi, unapotoka nje, unapoingia,^b

Na unapokuwa na ghadhabu dhidi yangu,^c

29 Kwa sababu ghadhabu yako dhidi yangu^d na mngurumo wako umefika masikioni mwangu.^e

Basi nitatia kulabu yangu puani mwako na lijamu yangu^f katikati ya midomo yako,

Nami nitakurudisha kupitia njia uliyotumia kuja.”

30 “Na hii ndiyo itakayokuwa ishara kwako:* Mwaka huu utakula mimea inayoota yenyewe;” na katika mwaka wa pili utakula nafaka inayochipuka kutoka katika mimea hiyo; lakini katika mwaka wa tatu utapanda mbegu na kuvuna, nawe utapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake.^g **31** Watu wa nyumba ya Yuda watakaoponyoka, wale wanaobaki,^h watatia mizizi chini na kuzaa matunda kwenda juu. **32** Kwa maana waliobaki watatoka Yerusalem na waokokaji wata-toka katika Mlima Sayuni.ⁱ Bi-

37:30 *Yaani, Hezekia. [#]Au “nafaka zilizozanguka na kuota zenyewe.”

SURA YA 37

a 2Fa 19:25, 26

b Met 5:21
Met 15:3
Ebr 4:13

c 2Fa 19:27, 28

d Zb 46:6
Isa 10:15
Isa 37:23

e Isa 36:4, 20

f Zb 32:9

g 2Fa 19:29-31

h Isa 1:9
Isa 10:20, 21

i 2Fa 19:4

Safu ya 2

a Isa 59:17
Yoe 2:18
Zek 1:14, 15

b Isa 10:24

c 2Nya 32:22
Isa 10:32

d 2Fa 19:32-34

e Isa 31:5

f Kum 32:27
1Sa 12:22
2Fa 20:6
Eze 36:22

g 1Fa 15:4

h 2Fa 19:35-37
2Nya 32:21

i Mwa 10:8, 11
Yon 1:2

j 2Fa 19:7, 28

k 2Nya 32:21

l Mwa 8:4

m Eze 4:1, 2

SURA YA 38

n 2Nya 32:24

o 2Fa 19:20
Isa 1:1

p 2Fa 20:1-3

dii ya Yehova wa majeshi itatenda hayo.^a

33 “Kwa hiyo Yehova anasema hivi kuhusu mfalme wa Ashuru:^b

“Hataingia katika jiji hili^c Wala hatapiga mshale humo

Wala kulikabili kwa ngao Wala kujenga boma la kulingira.”^d

34 ‘Atarudi kupitia njia aliyotumia kuja;

Hataingia katika jiji hili,’ asema Yehova.

35 ‘Nitalilinda jiji hili^e na ku-liokoa kwa ajili yangu^f mwenyewe

Na kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu.”^g

36 Na malaika wa Yehova akaenda na kuwau wanau-me 185,000 katika kambi ya Waashuru. Watu walipoamka asubuhi na mapema, waliona maiti zote hizo.^h **37** Basi Mfalme Senakeribu wa Ashuru akaondoka, akarudi Ninawiⁱ na kukaa huko.^j **38** Na alipokuwa akinama katika nyumba ya* Nisroki mungu wake, watoto wake mwenyewe wa kiume Adrameleki na Shareza, walimuua kwa upanga^k na kutoroka nchi ya Ararati.^l Na Esar-hadoni^m mwanawe akawa mfalme baada yake.

38 Katika siku hizo Hezekia akawa mgonjwa karibu afe.ⁿ Nabii Isaya^o mwana wa Amози akaja na kumwambia, “Yehova anasema hivi: ‘Wape maagizo watu wa nyumba yako, kwa maana utakufa; hutapona.’”^p **2** Ndipo Hezekia akaageuza uso wake kuelekea ukutani, akaanza kusali

37:38 *Au “hekalu la.”

hivi kwa Yehova: **3** “Nakushi, Ee Yehova, tafadhali, kumbuka^a jinsi ambavyo nimetembea mbele zako kwa uaminifu na kwa moyo kamili,^b nami nimetenda mambo mema machoni pako.” Kisha Hezekia akaanza kulia sana na kububujikwa na machozi.

4 Kisha neno la Yehova likamjia Isaya, likisema: **5** “Rudi ukamwambie Hezekia,^c ‘Yehova, Mungu wa Daudi babu yako anasema hivi: “Nimesikia sala yako.^d Nimeona machozi yako.^e Sasa ninakuongezea miaka 15 ya kuishi,^f **6** nami nitakuokoa wewe na jiji hili kutoka mikononi mwa mfalme wa Ashuru, nami nitalilinda jiji hili.^g **7** Hii ndiyo ishara kutoka kwa Yehova itakayokuonyesha kwamba Yehova atatimiza neno alilosema:^h **8** Nitafanya kivuli cha jua kinachoshuka kwenye ngazi* ya Ahazi kirudi nyuma hatua kumi.”””” Basi jua likarudi nyuma hatua kumi kwenye ngazi ambayo tayari lilikuwa limeshuka.

9 Haya ni maandishi ya* Mfalme Hezekia wa Yuda, aliposhikwa na ugonjwa na kupaona ugonjwa wake.

10 Nilisema: “Katikati ya maisha yangu Lazima niingie katika malango ya Kaburi.* Nitanyimwa miaka yangu iliyobaki.”

11 Nilisema: “Sitamwona Yah,* Yah katika nchi ya walio hai.^j

38:5 *Tnn., “katika siku zako.” **38:8** *Labda hatua hizo za ngazi zilitumiwa kuhesabu muda, kama saa ya kivuli. **38:9** *Au “Huu ni utungo wa.” **38:10** *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. **38:11** *”Yah” ni ufupisho wa jina Yehova.

SURA YA 38

a Ne 13:22
Zb 20:1-3
Ebr 6:10

b 2Nya 31:20, 21

c 2Fa 20:4-6

d Met 15:29
1Yo 5:14

e Zb 39:12
Zb 56:8

f Kum 32:39
1Sa 2:6

g 2Nya 32:22

h 2Fa 20:8-11

i Yos 10:12, 13

j Zb 6:5
Mhu 9:5

Safu ya 2

a Zb 146:4
Mhu 8:8

b Ayu 17:1

c Zb 39:10

d Zb 102:7

e Isa 59:11

f Zb 39:7

g Zb 39:12
Zb 119:82, 123

Sitawaona tena wanadamu Nitakapokuwa pamoja na wakaaji wa mahali ambapo kila kitu hukoma.

12 Makao yangu yameng’olewa na kuondolewa kwangu^a

Kama hema la mchungaji. Nimeukunja uhai wangu kama mfumaji wa nguo; Ananikata kabisa kama nyuzi za mtande.

Kuanzia mapambazuko mpaka usiku unaendelea kunimaliza.^b

13 Nimejituliza mpaka asubuhi.

Kama simba, anaendelea kuivunja mifupa yangu yote;

Kuanzia mapambazuko mpaka usiku unaendelea kunimaliza.^c

14 Ninaendelea kulia kama mbayuwauy au teleka;^{*d} Ninaendelea kulia kama njiwa.^e

Macho yangu yanatazama kileleni kwa uchovu:^f ‘Ee Yehova, ninataabika sana;

Uwe msaada wangu!”^g

15 Niseme nini?

Amezungumza nami na kutenda.

Nitatembea kwa unyenyekevu* miaka yangu yote Kwa sababu ya mateso yangu makali.[#]

16 ‘Ee Yehova, kila mwanadamu anaishi kwa mambo haya,*

Na katika mambo hayo

38:14 *Au labda, “korongo.” [#]Tnn., “Uwe dhamana yangu.” **38:15** *Au “ki-myakimya.” [#]Au “uchungu wa nafsi yangu.” **38:16** *Yaani, maneno na matendo ya Mungu.

kuna uhai wa roho
yangu.

Utaniponya na kunihifa-
dhi hai.^a

- 17** Tazama! Badala ya amani,
nilikuwa na uchungu
mwingi;

Lakini kwa sababu ulinipe-
nda sana,*

Uliniokoa kutokana na shi-
mo la maangamizi.^b

Umezitupa dhambi zangu
zote nyuma ya mgongo
wako.^{#c}

- 18** Kwa maana Kaburi* hali-
wezi kukutukuza,^d
Kifo hakiwezi kukusifu.^e
Wale wanaoshuka shimoni
hawawezi kuutumaini
uaminifu wako.^f

- 19** Walio hai, walio hai wana-
weza kukusifu,
Kama ninavyoweza leo hii.
Baba anaweza kuwapa
wanawe ujuzi kuhusu
uaminifu wako.^g

- 20** Ee Yehova, niokoe,
Nasi tutapiga mlibo
zangu kwa vinanda^h
Siku zote za maisha yetu
katika nyumba ya Ye-
hova.”ⁱ

21 Ndipo Isaya akasema:
“Leteni keki ya tini kavu zi-
lizoshinikizwa mlipake jipu
hilo, ili apone.”^j **22** Hezekia
alikuwa ameuliza: “Ni isha-
ra gani itakayonionyesha kwa-
mba nitapanda kwenda kati-
ka nyumba ya Yehova?”^k

39 Wakati huo mfalme
wa Babiloni, Merodak-
baladani mwana wa Bala-
dani alimtumia Hezekia barua

38:17 *Au “uliiipenda sana nafsi yan-
gu.” #Au “Umeziondoa dhambi zan-
gu zote kutoka mbele ya macho yako.”
38:18 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi,
uku. 2012.

SURA YA 38

a 1Sa 2:6
Ayu 33:28
Zb 71:20

b Zb 30:3
Zb 86:13
Yon 2:6

c Isa 43:25
Mik 7:18

d Zb 30:9

e Zb 6:5
Zb 115:17

f Mhu 9:5, 10

g Mwa 18:19
Kum 4:9
Yos 4:21-24

h Zb 30:11, 12

i 2Fa 20:5
Zb 84:2

j 2Fa 20:7

k 2Fa 20:8

Safu ya 2

SURA YA 39

a 2Nya 32:23

b 2Fa 20:5
2Fa 20:12, 13

c 2Nya 32:27

d 2Fa 20:14, 15

e 2Fa 24:11, 13
2Fa 25:13
2Nya 36:18
Da 1:1, 2

f 2Fa 20:16-18

g 2Fa 24:12
Da 2:49
Da 5:29

na zawadi,^a kwa maana alisi-
kia kwamba alikuwa mgonjwa
na sasa amepona.^b **2** Heze-
kia akawakaribisha kwa fu-
raha* na kuwaonyesha nyu-
mba yake yenye hazina^c—fe-
dha, dhahabu, mafuta ya zeri
na mafuta mengine yenye tha-
mani, ghala lake lote la silaha,
na kila kitu kilichokuwa kati-
ka hazina zake. Hakuna kitu
chochote ambacho Hezekia
hakuwaonyesha katika nyu-
mba yake mwenyewe[#] na kati-
ka milki yake yote.

3 Kisha nabii Isaya akaenda
kwa Mfalme Hezekia na ku-
muuliza: “Watu hawa walise-
ma nini, nao walitoka wapi?”
Hezekia akajibu: “Walitoka
katika nchi ya mbali, kuto-
ka Babiloni.”^d **4** Kisha akau-
liza: “Waliona nini katika nyu-
mba yako?”^e Hezekia akajibu:
“Waliona kila kitu katika nyu-
mba yangu.[#] Hakuna chocho-
te ambacho sikuwaonyesha
katika hazina zangu.”

5 Sasa Isaya akamwambia
Hezekia: “Sikia neno la Yeho-
va wa majeshi, **6** ‘Tazama!
Siku zinakuja, na vitu vyote
vilivyo katika nyumba yako*
na vitu vyote ambavyo maba-
bu zako wamehifadhi mpaka
leo hii vitapelekwa Babiloni.
Hakuna chochote kitakacho-
baki,’^e asema Yehova.^f **7** ‘Na
baadhi ya wana wako mwe-
nyewe utakaowazaa wachu-
kuliwa na kuwa maofisa wa
makao ya mfalme katika ju-
mba la mfalme wa Babiloni.’”^g

8 Ndipo Hezekia akamwa-
mbia Isaya: “Neno la Yehova

39:2 *Tnn., “akawashangilia.” #Au “ju-
mba lake mwenyewe la mfalme.” **39:4**
*Au “jumba lako la mfalme?” #Au “ju-
mba langu la mfalme.” **39:6** *Au “ju-
mba lako la mfalme.”

ambalo umesema ni jema.” Ki-sha akasema: “Kwa sababu ku-takuwa na amani na utulivu* wakati wa maisha yangu.”^{#a}

40 “Wafarijini, wafarijini watu wangu,” asema Mungu wenu.^b

2 “Zungumzeni na moyo wa* Yerusalemu, Na kulitangazia kwamba utumishi wake wa kulazi-mishwa umetimizwa, Kwamba hatia yake ime-lipwa.^c

Limepokea kutoka mkono-ni mwa Yehova malipo kamili[#] kwa ajili ya dha-mbi zake zote.”^d

3 Kuna mtu anayepaza sauti nyikani:

“Fungueni* njia ya Yehova!^e

Tengenezeni barabara kuu iliyonyooka^f inayopitia jangwani kwa ajili ya Mu-ngu wetu.^g

4 Kila bonde na liinuliwe, Na kila mlima na kilima kishushwe. Na ardhi yenye mashimo-mashimo itasawazishwa, Na ardhi yenye mawe-mawe itakuwa bonde tambarare.^h

5 Utukufu wa Yehova utafu-nuliwa,ⁱ Na wote wenye mwili* wa-taona pamoja,^j

Kwa maana kinywa cha Ye-hova kimesema hayo.”

6 Sikilizeni! Kuna mtu ana-yesema: “Tangaza!” Mwingine anauliza: “Nita-ngaze nini?”

39:8 *Au “ukweli.” [#]Tnn., “katika siku zangu.” **40:2** *Au “Lifarijini.” [#]Au “malipo maradufu.” **40:3** *Au “Tayari-sheni.” **40:5** *Au “wanadamu wote.”

SURA YA 39
a 2Fa 20:19

SURA YA 40

b Isa 49:13
Isa 51:3
2Ko 1:3, 4

c Zb 79:8, 9
Yer 31:34
Yer 33:8

d Yer 16:18
Da 9:11, 12

e Isa 35:8
Isa 57:14
Mal 3:1

f Isa 11:16

g Mt 3:1, 3
Mk 1:2-4
Lu 3:3-6
Yoh 1:23

h Isa 42:16

i Isa 24:15

j Isa 49:6
Isa 52:10

Safu ya 2

a Ayu 14:1, 2
Zb 90:5, 6

b Yak 1:11

c Zb 103:15, 16

d Isa 46:10
Ipe 1:24, 25

e Isa 52:7

f Isa 12:2
Isa 25:9

g Isa 53:1
Yoh 12:37, 38

h Isa 62:11
Ufu 22:12

i Isa 49:10
Eze 34:15, 16
Ipe 2:25

“Wote wenye mwili* ni ma-jani mabichi.

Upendo wao wote mshi-kamanifu ni kama ua la shambani.^a

7 Majani mabichi hukauka, Ua hunyauka,^b

Kwa sababu pumzi* ya Ye-hova hapuliza juu yake.^c Kwa hakika watu ni majani mabichi tu.

8 Majani mabichi hukauka, Ua hunyauka, Lakini neno la Mungu wetu linadumu milele.”^d

9 Panda juu ya mlima mrefu, Ewe mwanamke unaye-letea Sayuni habari njema.^e

Paza sauti yako kwa nguvu,

Ewe mwanamke unayeli-letea Yerusalemu habari njema.

Ipaze, usiogope.

Yatangazie majiji ya Yuda: “Tazameni Mungu wenu.”^f

10 Tazameni! Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atakuja kwa nguvu, Na mkono wake utatawala kwa ajili yake.^g

Tazameni! Anakuja na tha-wabu yake, Na malipo anayotoa yako mbele zake.^h

11 Atalitunza* kundi lake kama mchungaji.ⁱ Atawakusanya pamoja wanakondoo kwa mkono wake, Naye atawabeba kwenye kifua chake. Atawaongoza kwa upole

40:6 *Au “Wanadamu wote.” **40:7** *Au “roho.” **40:11** *Au “Atalichunga.”

- wale wanaonyonyesha watoto wao.^a
- 12** Ni nani amepima maji katika konzi ya mkono wake^b
Na kupima vipimo vya* mbingu kwa shubiri* ya mkono wake?
Ni nani ameyakusanya mavumbi ya dunia katika kipimio^c
Au kupima milima katika mizani
Na vilima katika mizani?
- 13** Ni nani ambaye amepima* roho ya Yehova, Na ni nani anayeweza kumfundisha akiwa mshauri wake?^d
- 14** Alishauriana na nani ili apate uelewaji, Au ni nani anayemfundisha njia ya haki, Au kumfundisha ujuzi, Au kumwonyesha njia ya uelewaji wa kweli?^e
- 15** Tazameni! Mataifa ni kama tone kutoka katika ndoo, Naye huyaona kuwa kama mavumbi memamba juu ya mizani.^f
Tazameni! Anaviinua visiwa kama mavumbi laini.
- 16** Hata Lebanoni haitoshi kufanya moto uendelee kuwaka,*
Na wanyama wake wa mwi-tuni hawatoshi kwa ajili ya dhabihu ya kuteke-tezwa.
- 17** Mbele zake mataifa yote

40:12 *Au "ukubwa wa." #Ni urefu kuanzia kidole gumba hadi kidole kido-go, kiganja kikiwa kimepanuliwa. Angalia Nyongeza B14. 40:13 *Au labda, "ameielewa." 40:16 *Au "haiwezi kuan-da kuni za kutosha."

SURA YA 40

a Mwa 33:13
1Pe 5:2, 3

b Met 30:4

c Ayu 38:4, 5

d Ayu 36:22, 23
Ro 11:34
1Ko 2:16

e Zb 147:5

f Zb 62:9

Safu ya 2

a Da 4:35

b Isa 41:11, 12

c Kut 8:10
Zb 86:8
Yer 10:6, 7

d Kum 4:15, 16
Mdo 17:29

e Zb 115:4-8

f Isa 44:14, 15

g Isa 41:7
Isa 46:6, 7
Yer 10:3, 4

h Zb 19:1
Ro 1:20

i Isa 66:1

j Isa 44:24
Yer 10:12
Zek 12:1

- ni kama kitu kisichokuwepo:^a
Anayaona kuwa si kitu, kama ubatili.^b
- 18** Mnaweza kumlinganisha Mungu na nani?^c
Mnaweza kumfananisha na nini?^d
- 19** Fundi hutengeneza sanamu,*
Mfua chuma huifunika kwa dhahabu,^e
Naye huitengenezea miku-fu ya fedha.
- 20** Huchagua mti fulani uwe mchango wake,^f
Mti ambao hautaoza. Humtafuta fundi stadi Ili atengeneze sanamu ya kuchongwa ambayo hai-taanguka.^g
- 21** Je, hamjui?
Je, hamjasikia?
Je, hamkuambiwa tangu mwanzoni?
Je, hamjalewa tangu misingi ya dunia ilipo-wekwa?^h
- 22** Kuna Yule anayekaa juu ya duara ya* dunia,ⁱ
Na wakaaji wake ni kama panzi.
Anazitandaza mbingu kama wavu laini,
Naye huzitandaza kama hema la kuishi.^j
- 23** Huwafanya maofisa wakuu kuwa si kitu
Na kuwafanya waamuzi* wa dunia wawe ubatili.
- 24** Bado hawajapandwa, Bado hawajatiwa ardhini, Bado shina lao halijatia mizizi ardhini,

40:19 *Au "sanamu ya kuyeyushwa." 40:22 *Au "tufe la." 40:23 *Au "wata-wala."

- Nao hupuliziwa na kuka, Na upepo huwapeperusha mbali kama majani makavu.^a
- 25** “Mnaweza kunifananisha na nani ili niwe sawa naye?” auliza Yule Mta-katifu.
- 26** “Inueni macho yenu mbinguni mwone. Ni nani aliyevumba vitu hivi?^b Ni Yule anayelileta nje jeshi lao kwa hesabu; Huziita zote kwa majina.^c Kwa sababu ya nguvu zake nyingi zenye msukumo na nguvu zake zenye kuogopesha,^d Hakuna hata moja inayokosekana.
- 27** Ewe Yakobo, kwa nini unasema, na ewe Israeli, kwa nini unatangaza, ‘Njia yangu imefichwa kutoka kwa Yehova, Nami sipati haki kutoka kwa Mungu?’^e
- 28** Je, hujui? Je, hujasikia? Yehova, Muumba wa mii-sho ya dunia, ni Mungu kwa umilele wote.^f Yeye hachoki kamwe wala haishiwi na nguvu.^g Uelewaji wake hauchungu-ziki.^h
- 29** Yeye humpa nguvu mtu aliyechoka Na kuwapa uwezo kamili wale wasio na nguvu.ⁱ
- 30** Wavulana watachoka na kuishiwa na nguvu, Na vijana watajikwaa na kuanguka,
- 31** Lakini wale wanaomtu-

40:28 *Au “hauwezi kueleweka.”
40:29 *Au “nguvu zenye msukumo.”

SURA YA 40

a 1Fa 21:20, 21
2Fa 10:10, 11
Yer 22:24, 30

b Zb 102:25

c Zb 147:4

d Zb 89:13

e Isa 49:14
Eze 37:11

f Mwa 21:33
Zb 90:2
Yer 10:10
1Ti 1:17

g Zb 121:4
Isa 27:3

h Zb 139:4, 6
Zb 147:5
Isa 55:9
Ro 11:33
1Ko 2:16

i Zb 29:11
Isa 40:26
Flp 4:13
Ebr 11:33, 34

Safu ya 2

a Zb 103:5

b 1Fa 18:46
Zb 84:7

SURA YA 41

c Isa 41:21

d Isa 44:28
Isa 46:11
Ufu 16:12

e Isa 45:1

f Isa 43:10
Isa 44:6
Isa 48:12
Ufu 1:8

g Isa 46:4
Mal 3:6
Yak 1:17

maini Yehova watapata nguvu tena.

Watapaa juu kwa mabawa kama tai.^a

Watakimbia na hawataishiwa na nguvu;

Watatembea na hawatachoka.^b

41 “Nisikilizeni mkiwa kima, * enyi visiwa; Mataifa na yapate nguvu tena.

Na yakaribie; kisha yao- ngee.^c

Na tukutane pamoja kwenye hukumu.

2 Ni nani amemwinua mtu kutoka mashariki, *^d Akimwita katika uadilifu aje miguuni Pake,^e

Ili amkabidhi mataifa Na kumfanya awatiishe wafalme?^e

Ambaye anawafanya wawe mavumbi mbele ya upanga wake,

Kama majani makavu yanayopeperushwa na upepo mbele ya upinde wake?

3 Anawafuatia, anapita bila kuzuiwa Kwenye njia ambazo miguu yake haijawahi kupita.

4 Ni nani ametenda na kufanya jambo hili, Kuviita vizazi tangu mwanzoni?

Mimi, Yehova, Ndiye wa Kwanza;^f

Na kwa wale wa mwisho mimi ni yuleyule.^g

5 Visiwi vimeona hivyo na kuogopa.

41:1 *Au “Nyamazeni mbele zangu.”
41:2 *Au “upande wa mapambazuko ya jua.”^a Yaani, ili amtumikie Yeye.

Miisho ya dunia ilianza kutetemeka.

Wanakaribia na kuja mbele.

6 Kila mmoja anamsaidia mwenzake

Na kumwambia ndugu yake: “Uwe imara.”

7 Kwa hiyo fundi anamwimarisha mfua chuma;^a

Yule anayelainisha kwa nyundo ya chuma Anamwimarisha yule agogaye kwenye fuawe.

Anasema hivi kuhusu lehemu: “Ni nzuri.”

Kisha inapigiliwa misumari ili isianguke.

8 “Lakini wewe ni mtumishi wangu, Ee Israeli,^b

Wewe niliyekuchagua, Ee Yakobo,^c

Uzao wa* rafiki yangu Abrahamu,^d

9 Wewe, niliyekuchukua kutoka kwenye miisho ya dunia,^e

Na wewe, niliyekuita kutoka sehemu zake za mbali zaidi.

Nilikuambia, ‘Wewe ni mtumishi wangu;’^f

Nimekuchagua wewe; sija-kukataa.^g

10 Usiogope, kwa maana mimi niko pamoja nawe.^h

Usihangaiki, kwa maana mimi ni Mungu wako.ⁱ

Nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia,^j

Nitakushika kwelikweli kwa mkono wangu wa kuume wa uadilifu.’

11 Tazama! Wale wote wanaowaka hasira dhidi yako wataaibishwa na kufedheheshwa.^k

SURA YA 41

a Isa 44:12
Isa 46:6

b Kut 19:5, 6
Law 25:42

c Kum 7:6
Zb 33:12

d 2Nya 20:7
Yak 2:23

e Zb 107:2, 3

f Isa 43:10

g Isa 12:22
Yer 33:25, 26

h Kum 20:1
Zb 46:1
Ro 8:31

i Isa 60:19, 20

j Kum 33:27
Zb 115:9

k Isa 45:24

Safu ya 2

a Isa 40:17
Isa 60:12

b Isa 54:17

c Kum 33:29

d Kum 7:7

e Isa 43:14
Isa 47:4

f Mik 4:13

g Isa 25:9

h Isa 12:6

Wale wanaopigana nawe watafanywa kuwa si kitu na wataangamia.^a

12 Utawatafuta watu wanaopambana nawe, lakini hutawapata;

Watu wanaopigana nawe watakuwa kama kitu kisichokuwepo, watakuwa si kitu kabisa.^b

13 Kwa maana mimi, Yehova Mungu wako, ninaushika kwa nguvu mkono wako wa kulia,

Mimi ninayekuambia, ‘Usiogope. Nitakusaidia.’^c

14 Usiogope, wewe mnyoo* Yakobo,^d

Ninyi watu wa Israeli, nitawasaidia,” asema Yehova, Mkombozi wenu,^e Mtakatifu wa Israeli.

15 “Tazama! Nimekufanya uwe kifaa cha kupuria,^f Kifaa kipya cha kupuria chenye meno yenye makali pande mbili.

Utaikanyaga-kanyaga mili-ma na kuipondaponda Na kuvifanya vilima viwe kama makapi.

16 Utawapepeta, Na upepo utawapeperusha mbali;

Dhoruba ya upepo itawatawanyanya.

Utashangilia katika Yehova,^g

Nawe utajigamba katika Mtakatifu wa Israeli.”^h

17 “Wenye uhitaji na maskini wanatafuta maji, lakini hayapo.

41:14 *Yaani, mtu wa hali ya chini asiye na ulinzi.

Ulimi wao umekauka kwa sababu ya kiu.^a

Mimi, Yehova, nitawajibu.^b

Mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha.^c

18 Nitafanya mito itiririke kwenye vilima visivyo na kitu^d

Na chemchemi katika mabonde tambarare.^e

Nitaigeuza nyika kuwa dimbwi la maji lenye matete

Na nchi isiyo na maji kuwa chemchemi za maji.^f

19 Nitapanda mwerezi jangwani,

Mshita na mhadasi na msonbari,^g

Nitapanda mberoshi katika jangwa tambarare,

Pamoja na mtidhari na mvinje,^h

20 Ili watu wote waone na kujua

Wakaze fikira na kuelewa Kwamba mkono wa Yehova umetenda hayo,

Na Mtakatifu wa Israeli ameliumba jambo hilo.”ⁱ

21 “Leteni kesi yenu,” asema Yehova.

“Toeni hoja zenu,” asema Mfalme wa Yakobo.

22 “Leteni ushahidi na mtuambie mambo yatakayotendeka.

Tuambieni kuhusu mambo ya zamani,^{*}

Ili tuyatafakari[#] na kujua matokeo yake

Au mtungazie mambo yanayokuja.^j

23 Tuambieni mambo yataka-yotokea wakati ujao,

SURA YA 41

a Kum 28:48
Amo 8:11

b Isa 30:19
Isa 55:1

c Zb 94:14
Isa 42:16
Ebr 13:5

d Isa 30:25

e Yoe 3:18

f Zb 107:35

g Isa 32:14, 15
Isa 60:21

h Isa 51:3
Isa 55:13

i Eze 39:28

j Isa 42:9
Isa 46:9, 10
Isa 48:5

Safu ya 2

a Isa 44:6, 7

b Yer 10:5

c Isa 44:10
Yer 10:14, 15

d Kum 7:26
Kum 27:15
Zb 115:4, 8

e Isa 44:28
Isa 45:1
Yer 51:28, 29

f Isa 46:11
Ufu 16:12

g Mik 7:10

h Isa 43:9
Isa 44:7
Isa 45:21

i Hab 2:18, 19

j Isa 43:10

k Ezz 1:1, 2
Isa 40:9

Ili tujue kwamba ninyi ni miungu.^a

Naam, fanyeni jambo, zuri au baya,

Ili tushangae tutakapoliona.^b

24 Tazameni! Ninyi ni kitu kisichokuwepo,

Na mafanikio yenu si kitu.^c Mtu yeyote anayewachagua ninyi anachukiza.^d

25 Nimemwinua mtu kutoka kaskazini, naye atakuja,^e

Kutoka upande wa mapambazuko ya jua,^{*f}

atakayeliitia jina langu.

Atawakanyaga-kanyaga watawala[#] kana kwamba wao ni udongo,^g

Kama mfinyanzi anayeukanyaga-kanyaga udongo wenye maji.

26 Ni nani aliyesema jambo hilo tangu mwanzoni, ili tulijue,

Au kutoka nyakati za zamani, ili tuseme, ‘Yeye anasema kweli’?^h

Kwa kweli, hakuna mtu aliyelitangaza!

Hakuna mtu aliyelisema! Hakuna mtu aliyesikia lote kutoka kwenu!”ⁱ

27 Nilikuwa wa kwanza kumwambia Sayuni: “Tazama! Wako hapa!”^j

Na kwa Yerusalemu nitaamtama mtu anayepeleka habari njema.^k

28 Lakini niliendelea kutazama, na hapakuwa na mtu;

Hakukuwa na mtu yeyote kati yao ambaye angetoa ushauri.

Nami niliendelea kuwao- mba wanijibu.

28 Lakini niliendelea kutazama, na hapakuwa na mtu; Hakukuwa na mtu yeyote kati yao ambaye angetoa ushauri. Nami niliendelea kuwao- mba wanijibu.

41:22 *Tnn., “kwanza.” #Au “tuyaelekezee moyo wetu.”

41:25 *Au “mashariki.” #Au “watawala wasaidizi.”

29 Tazameni! Wote ni udanganyifu.*
Kazi zao si kitu.
Sanamu zao za chuma[#] ni upepo na ubatili.^a

42 Tazama! Mtumishi wangu,^b ninayemtegemeza!

Mchaguliwa wangu,^c ambaye nime mkubali!^{*d}
Nimeitia roho yangu ndani yake;^e
Atayaleta mataifa haki.^f

2 Hatalia kwa sauti wala kupaza sauti yake,
Naye hatafanya sauti yake isikike barabarani.^g

3 Hataponda tete lililovunjika,
Wala hatazima utambi unaofifia.^h
Ataleta haki kwa uaminifu.ⁱ

4 Hatafifia wala kupondwa mpaka atakapoimarisha haki duniani;^j
Na visiwa vinaendelea kungojea sheria* yake.

5 Hivi ndivyo anavyosema Mungu wa kweli, Yehova, Muumba wa mbingu na Mkuu aliyezetandaza,^k
Yule aliyezetandaza dunia na mazao yake,^l
Yule anayewapa pumzi watu waliomo.^m
Na kuwapa roho wale wanaotembea humo.ⁿ

6 “Mimi, Yehova, nimekuita katika uadilifu;
Nimekushika mkono wako. Nitakulinda na kukutoa uwe agano kwa ajili ya watu^o

41:29 *Au “kitu kichokuwepo.” [#]Au “Sanamu zao za kuyeyushwa.” 42:1 *Au “nafsi yangu imemkubali.” 42:4 *Au “mafundisho.”

SURA YA 41

a Zb 115:4-8
Isa 44:9
1Ko 8:4

SURA YA 42

b Isa 52:13
c Isa 49:7
Lu 9:35
d Mt 3:17
Yoh 6:27
2Pe 1:17
e Isa 61:1
Mt 3:16
f Mt 12:15-18
g Zek 9:9
Mt 12:16, 19
h Mt 11:28, 29
Ebr 2:17
i Isa 11:3, 4
Mt 12:20
Yoh 5:30
Ufu 19:11
j Isa 9:7
Isa 49:8
k Isa 40:22, 26
l Yer 10:12
m Mwa 2:7
Mdo 17:24, 25
n Ayu 12:10
o Isa 49:8

Safu ya 2

a Isa 49:6
Lu 2:29-32
Yoh 8:12
b Isa 35:5
c Isa 61:1
1Pe 2:9
d Kut 34:14
e Isa 41:23
Isa 43:19
2Pe 1:21
f Zb 96:1
Zb 98:1
Ufu 14:3
g Isa 44:23
h Isa 51:5
i Isa 35:1
j Mwa 25:13
Isa 60:7
k Zb 22:27
Isa 24:15
Isa 66:19
l Isa 59:17

Na uwe nuru kwa mataifa,^a

7 Ili uyafungue macho yaliyopofuka,^b
Ili umtoe mfungwa katika gereza lililo chini ya ardhi
Na wale wanaoketi gizani kutoka gerezani.^c
8 Mimi ni Yehova. Hilo ndilo jina langu;
Simpi yeyote utukufu wangu,*

Wala kuzipa sanamu za kuchongwa sifa yangu.^d

9 Tazameni, mambo ya kwanza yametokea;
Sasa ninatangaza mambo mapya.

Kabla hayajatokea, ninawaambia kuyahusu.^e

10 Mwimbieni Yehova wimbo mpya,^f
Sifa yake kutoka kwenye miisho ya dunia,^g

Ninyi mnaoshuka baharini na pia vyote vinavyojaza,

Ninyi visiwa na wakaaji wake.^h

11 Nyika na majiji yake na yapaze sauti yao,ⁱ
Makao ambamo Kedari anaishi.^j

Wale wanaokaa kwenye jabali na wapige vigelegele kwa shangwe;

Na wapaze sauti kutoka kwenye vilele vya milima.

12 Na wamtukuze Yehova Na watangaze sifa zake katika visiwa.^k

13 Yehova atatoka kama mwanamume hodari.^l

42:8 *Au “Sishiriki utukufu wangu na yeyote.”

- Ataamsha bidii yake kama shujaa.^a
 Atapaza sauti, naam, atapiga kelele za vita;
 Ataonyesha kwamba ana nguvu kuliko maadui wake.^b
- 14** “Nimenyamaza kwa muda mrefu.
 Niliendelea kukaa kimya na kujizuia.
 Kama mwanamke anayezaa,
 Nitalia kwa uchungu, nita-hemahema, na kutweta wakati uleule.
- 15** Nitaiharibu milima na vilima
 Na kukausha kabisa majani yake yote.
 Nitaibadili mito iwe visiwa*
 Na kuyakausha kabisa madimbwi ya maji yenye matete.^c
- 16** Nitawaongoza vipofu kwenye njia wasiyojua^d
 Na kuwafanya watembe kwenye vijia wasivyo-vijua.^e
 Nitabadili giza lililo mbele yao liwe nuru^f
 Na kubadili eneo lenye mawemawe kuwa nchi tambarare.^g
 Hivyo ndivyo nitakavyo-watendea, nami sitawaacha.”
- 17** Watarudishwa nyuma na kuaibishwa kabisa,
 Wale wanaotumaini sanamu za kuchongwa,
 Wale wanaoziambia sanamu za chuma:* “Ninyi ni miungu yetu.”^h
- 18** Sikilizeni, ninyi viziwi;

42:15 *Au “maeneo ya pwani.” 42:17
 *Au “sanamu za kuyeyushwa.”

SURA YA 42

a Kut 15:3

b 1Sa 2:10

c Zb 107:33
Isa 44:27
Isa 50:2d Isa 29:18
Isa 35:5
Yer 31:8

e Isa 30:21

f Isa 60:1, 20

g Isa 40:4

h Isa 44:10, 11
Isa 45:16

Safu ya 2

a Isa 6:9, 10
Isa 43:8b Isa 56:10
Yer 4:22
Eze 12:2

c Eze 33:31

d Kum 28:15, 33
Yer 50:17

e Zb 102:19, 20

f Kum 28:29, 52

Tazameni na mwone, ninyi vipofu.^a

- 19** Ni nani aliye kipofu isipokuwa mtumishi wangu,
 Aliye kiziwi sana kama mjumbe ninayemtuma?
 Ni nani aliye kipofu sana kama yule ambaye amethawabishwa,
 Aliye kipofu sana kama mtumishi wa Yehova?^b
- 20** Unaona mambo mengi, lakini huendelei kukaa macho.
 Unafungua masikio yako, lakini husikilizi.^c
- 21** Kwa sababu ya uadilifu wake,
 Yehova amependezwa kuitukuza sheria* na kuifanya iwe na utukufu.
- 22** Lakini watu hawa ni watu walioporwa na kutekwa nyara;^d
 Wote wamenaswa katika mashimo na kufichwa magerezani.^e
 Wameporwa na hakuna yeyote wa kuwaokoa,^f
 Nao wametekwa nyara na hakuna yeyote wa kusema: “Warudisheni!”
- 23** Ni nani kati yenu atakayesikia jambo hili?
 Ni nani atakayetega sikio na kusikiliza kwa ajili ya wakati ujao?
- 24** Ni nani aliyemtia Yakobo mikononi mwa watekaji nyara
 Na Israeli mikononi mwa waporaji?
 Je, si Yehova, Yule ambaye tumemtendea dhambi?
 Walikataa kutembea katika njia Zake,

42:21 *Au “mafundisho.”

Nao hawakutii sheria*
Yake.^a

- 25 Basi Yeye akaendelea kumwagwagia ghadhabu, Hasira yake na ghadhabu ya vita.^b

Iliteketeza kila kitu kumzunguka, lakini hakulikazia jambo hilo fikira.^c

Iliwaka dhidi yake, lakini hakulitia jambo hilo moyoni.^d

- 43 Sasa hivi ndivyo anavyosema Yehova, Muumba wako, Ee Yakobo, Yule aliyekuumba, Ee Israeli:^e

“Usiogope, kwa maana nimekukomboa.^f

Nimekuita kwa jina lako. Wewe ni mali yangu.

- 2 Unapopita katika maji, nitakuwa pamoja nawe,^g Na unapopita katika mito, haitafurika na kukufunika.^h

Unapotembea katika moto, hutateketea, Wala mwali wa moto hau-takuunguza.

- 3 Kwa maana mimi ni Yehova Mungu wako, Mtakatifu wa Israeli, Mwo-kozi wako.

Nimeitoa Misri kuwa fidia kwa ajili yako, Ethiopia na Seba badala yako.

- 4 Kwa sababu ulikuwa mwenye thamani machoni pangu,ⁱ

Uliheshimiwa, nami nimekupenda.^j

Basi nitawatoa watu bada-la yako

SURA YA 42

a Amu 2:12, 14
2Nya 15:3, 6
Zb 106:41

b Kum 32:22
Nah 1:6

c Isa 9:13
Yer 5:3
Ho 7:9

d Isa 57:11

SURA YA 43

e Zb 100:3
Isa 43:15
Isa 44:2, 21

f Isa 44:23
Yer 50:34

g Kut 14:29

h Yos 3:15, 16
2Fa 2:8

i Kut 19:5, 6

j Kum 7:8
Yer 31:3

Safu ya 2

a Isa 41:10
Isa 44:2
Yer 30:10

b Kum 30:1-3
Zb 106:47
Isa 66:20
Eze 36:24
Mik 2:12
Zek 8:7

c Yer 3:18

d Yer 31:8

e Yer 33:16

f Zb 100:3
Isa 29:23

g Isa 6:9, 10
Isa 42:18, 19

h Isa 41:1

i Isa 41:21, 22
Isa 44:7

j 1Fa 18:24, 25

k Mdo 1:8
Ufu 1:5

l Kum 4:37

Na mataifa badala ya uhai wako.*

- 5 Usiogope, kwa maana nipo pamoja nawe.^a Nitauleta uzao wako* kutoka mashariki

Na kukukusanya kutoka magharibi.^b

- 6 Nitaiambia kaskazini, ‘Watoe!’^c

Na kusini, ‘Usiwazuie.

Walete wanangu kutoka mbali, na mabinti wangu kutoka kwenye miisho ya dunia,^d

- 7 Kila mtu anayeitwa kwa jina langu^e

Na niliyemuumba kwa ajili ya utukufu wangu,

Ambaye nimemuumba na kumtokeza.^f

- 8 Waleteni watu walio vipofu, ingawa wana macho, Na walio viziwi, ingawa wana masikio.^g

- 9 Mataifa yote na yakusanyike mahali pamoja, Na watu wakusanyike pamoja.^h

Ni nani kati yao anayeweza kutangaza haya?

Au, je, wanaweza kutufanya tusikie mambo ya kwanza?^{*i}

Na watoe mashahidi wao ili kuthibitisha kwamba wanasema ukweli,

Au acha wasikie na kusema, ‘Ni ukweli!’^j

- 10 “Ninyi ni mashahidi wangu,”^k asema Yehova, “Naam, mtumishi wangu ambaye nimemchagua,^l

43:4 *Au “nafsi yako.” 43:5 *Tnn., “Nitauleta mbegu yako.” 43:9 *Labda ni mambo yatakayotokea kwanza wakati ujao.

- Ili mjue na kuwa na imani kwangu*
Na mwelewe kwamba mimi ni yuleyule.^a
Kabla yangu hakuna Mungu aliyefanyizwa, Na baada yangu hakutakuwa na mwingine.^b
- 11** Mimi—mimi ni Yehova,^c na zaidi yangu hakuna mwokozi.”^d
- 12** “Mimi ndiye niliyetangaza na kuokoa na kujulisha Kulipokuwa hakuna mungu wa kigeni miongoni mwenu.^e
Basi ninyi ni mashahidi wangu,” asema Yehova, “nami ni Mungu.^f
- 13** Pia, mimi ni yuleyule siku-zote;^g
Na hakuna yeyote anayeweza kunyakua chochote kutoka mkononi mwangu.^h
Ninapotenda, ni nani anayeweza kunizuia?”ⁱ
- 14** Yehova, Mkombozi wenu,^j Mtakatifu wa Israeli,^k anasema hivi:
“Nitatuma ujumbe huko Babiloni kwa ajili yenu na kuyashusha makomeo yote ya malango,^l
Na Wakaldayo, katika meli zao, watalia kwa sababu ya mateso.^m
- 15** Mimi ni Yehova, Mtakatifu wenu,ⁿ Muumba wa Israeli,^o Mfalme wenu.”^p
- 16** Yehova anasema hivi:
Yule anayetengeneza njia baharini
Na mahali pa kupita hata katika maji yenye msukuko,^q

SURA YA 43

a Isa 41:4

b Isa 44:8

c Kum 6:4

d Isa 12:2
Ho 13:4
1Ti 2:3
Yud 25

e Kum 32:12

f Isa 46:9, 10

g Isa 41:4
Ufu 1:8

h Kum 32:39

i Isa 14:27
Da 4:35j Isa 44:6
Isa 63:16

k Isa 54:5

l Isa 45:1, 2

m Yer 50:10

n Zb 89:18

o Isa 43:1

p Kum 33:5
Zb 74:12
Isa 33:22
Ufu 11:17q Kut 14:16
Yos 3:13

Safu ya 2

a Kut 15:4

b Yer 51:39

c Isa 42:9

d Isa 11:16
Isa 40:3

e Isa 41:18

f Isa 41:17
Yer 31:9g Zb 33:12
Isa 41:8
1Pe 2:9

h Isa 60:21

i Isa 64:7

j Yer 2:5
Ho 7:10
Mik 6:3

k Isa 66:3

- 17** Yule anayelivuta gari la vita na farasi,^a
Jeshi pamoja na mashujaa hodari:
“Watalala chini na hawa-taamka.^b
Watazimwa, watazimwa mara moja kama utambi unaowaka.”
- 18** “Msikumbuke mambo ya kwanza,
Wala msifikirie sana mambo ya zamani.
- 19** Tazameni! Ninatenda jambo jipya;^c
Hata sasa linachipuka.
Je, hamlitambui?
Nitatengeneza njia nyikani^d
Na mito jangwani.^e
- 20** Mnyama wa mwituni ataniheshimu,
Mbwanwitu na mbuni,
Kwa maana ninatokeza maji nyikani,
Mito jangwani,^f
Ili watu wangu wanywe, naam, mchaguliwa wangu,^g
- 21** Watu niliojiambia Ili watangaze sifa zangu.^h
- 22** Lakini hujaniita mimi, Ee Yakobo,ⁱ
Kwa sababu ulichoshwa nami, Ee Israeli.^j
- 23** Hujaniletea kondoo kwa ajili ya dhahabu zako nzima za kuteketezwa
Wala kunitukuza kwa dhahabu zako.
Sijakulazimisha uniletee zawadi,
Wala sijakuchosha kwa kudai ubani.^k
- 24** Hukuninunulia utete wenyewe manukato kwa pesa zako,

Wala hukuniridhisha kwa mafuta ya dhabihu zako.^a

Badala yake, umenilemea kwa dhambi zako Na kunichosha kwa maovu yako.^b

- 25 Mimi, mimi ndiye ninayeyafuta kabisa makosa*^c yako kwa ajili yangu,^d Nami sitazikumbuka dhambi zako.^e

- 26 Nikumbushe; na tukutane ili tufanye kesi; Toa hoja zako ili kuthibitisha kwamba unasema ukweli.

- 27 Babu yako wa kwanza alitenda dhambi, Na wasemaji* wako mwenyewe wameniasi.^f

- 28 Kwa hiyo nitawatia unajisi wakuu wa mahali patakatifu, Nami nitamtoa Yakobo aangamizwe Na kumfanya Israeli atukanwe.^g

- 44** "Sasa sikiliza, Ee Yakobo mtumishi wangu, Nawe, Ee Israeli, ambaye nimekuchagua.^h

- 2 Hivi ndivyo anavyosema Yehova, Muumba wako, Yule aliye-kutokeza,ⁱ Ambaye amekusaidia tangu ulipokuwa tumboni:* 'Usiogope, mtumishi wangu Yakobo,^j Na wewe, Yeshuruni,^k ambaye nimekuchagua.

43:25 *Au "matendo yako ya uasi."
43:27 *Labda hawa ni walimu wa Sheria. 44:2 *Au "tangu ulipozaliwa."
#Maana yake "Mnyoofu," jina la heshima la Israeli.

SURA YA 43

a Law 3:14-16

b Isa 1:14, 15

c Isa 1:18
Yer 50:20

d Zb 25:7
Zb 79:8, 9
Eze 20:9

e Yer 31:34

f Isa 28:7
Yer 5:31

g Zb 79:4
Zb 137:3

SURA YA 44

h Mwa 17:1, 7
Mwa 35:10, 11
Isa 41:8

i Isa 43:1
Isa 44:21

j Isa 41:10
Yer 30:10

k Kum 32:15
Kum 33:5, 26

Safu ya 2

a Isa 41:17

b Isa 32:14, 15

c Isa 61:11

d Zek 13:9

e Kum 33:5
Isa 33:22

f Kut 6:6
Yer 50:34

g Isa 41:4
Isa 48:12
Ufu 22:13

h Kum 4:35, 39
Isa 43:10

i Isa 46:9

j Isa 43:9
Isa 45:21

k Isa 41:10

- 3 Kwa maana nitammimonia maji mwenye kiu*^a Na kumimina vijito vina-vyotiririka kwenye ardhi iliyokauka.

Nitaimimina roho yangu juu ya uzao wako*^b Na baraka yangu juu ya wazao wako.

- 4 Nao watachipuka kama majani mabichi,^c Kama mierebi kando ya vijito vya maji.

- 5 Mtu mmoja atasema: "Mimi ni mali ya Yehova."^d

Mwingine atajiita kwa jina la Yakobo,

Na mwingine ataandika kwenye mkono wake: "Mali ya Yehova."

Naye atalichukua jina la Israeli.'

- 6 Yehova, Mfalme wa Israeli^e na Mkombozi wake,^f

Yehova wa majeshi, anasema hivi:

'Mimi ndiye wa kwanza na mimi ndiye wa mwisho.^g Hakuna Mungu ila mimi.^h

- 7 Ni nani aliye kama mimi?ⁱ Na aseme kwa sauti, atangaze, na kunithibitishia!^j

Tangu nilipowatokeza watu wa zamani za kale, Na waseme mambo yatakayokuja

Na yale yatakayotokea.

- 8 Msiogope, Wala msilemazwe na woga.^k

Je, sikumwambia kila mmoja wenu mapema na kutangaza jambo hilo?

44:3 *Au "nitaimimonia maji nchi yenye kiu." #Tnn., "mbegu yako."

Ninyi ni mashahidi wangu.^a
Je, kuna Mungu zaidi ya-
ngu?

Hapana, hakuna Mwamba
mwingine;^b simjui mwi-
ngine.”

9 Wale wote wanaotenge-
neza sanamu za
kuchongwa hawana tha-
mani yoyote,

Na vitu wanavyovipenda
sana havitakuwa na fai-
da yoyote.^c

Vikiwa kama mashahidi
wao, havioni* chochote
wala havijui chochote,^d

Basi waliovitengeneza vitu
hivyo wataaibishwa.^e

10 Ni nani anayeweza ku-
tengeneza mungu au
sanamu ya chuma*
Ambayo haina faida

yoyote?^f

11 Tazameni! Wenzake wote
wataaibishwa!^g

Mafundi ni wanadamu tu.
Wote na wakusanyike na
kusimama.

Watashikwa na hofu na
kuaibishwa pamoja.

12 Mhunzi hutengeneza sa-
namu ya chuma kwenye
makaa kwa kifaa chake.*
Anaiunda kwa nyundo,
Anaitengeneza kwa mkono
wake wenye nguvu.^h

Kisha anahisi njaa na kui-
shiwa na nguvu;
Hanywi maji na anachoka.

13 Mchongaji wa mbao hui-
nyoosha kamba ya
kupimia, huchora
umbo akitumia cho-
kaa nyekundu.

44:9 *Yaani, sanamu. **44:10** *Au “sa-
namu ya kuyeyushwa.” **44:12** *Au
“tezo yake.”

SURA YA 44

a Isa 43:10

b Kum 32:4
2Sa 22:32

c Amu 10:14
1Fa 18:26
1Ko 8:4

d Zb 115:4, 5

e Yer 51:17

f Yer 10:5
Mdo 19:26

g 1Sa 5:3, 7

h Isa 40:19
Isa 41:7
Isa 46:6

Safu ya 2

a Kut 20:4
Kum 4:15, 16
Mdo 17:29

b Kum 27:15

c Isa 40:20
Yer 10:3

d Kut 20:4, 5
Law 26:1
Hab 2:18, 19

e Isa 37:37, 38
Isa 45:20
Isa 46:7

f Yer 10:8, 14
Ro 1:21-23

Huchonga sanamu kwa
patasi na kuchora kwa
bikari.

Anaichonga kwa umbo la
mwanadamu,^a

Kwa uzuri wa mwanadamu,
Ili ikae katika nyumba.*^b

14 Kuna mtu ambaye kazi
yake ni kukata mierezi.
Huchagua mti wa aina fu-
lani, mwaloni,

Naye huuacha uwe imara
kati ya miti ya msituni.^c

Hupanda mlaursi, na
mvua huufanya ukue.

15 Kisha unakuwa kuni
zinazotumiwa na mwa-
nadamu kuwasha moto.
Huchukua baadhi yake ili
aote moto;

Huwasha moto na kuoka
mkate.

Lakini pia hutengeneza
mungu na kumwabudu.

Huutengeneza kuwa sana-
mu ya kuchongwa, na
kuiinamia.^d

16 Nusu yake huiteketeza
motoni;

Kwa nusu hiyo huchoma
nyama anayokula, naye
hushiba.

Pia huota moto na kusema:
“Aha! Ninahisi joto ninapo-
tazama moto.”

17 Lakini sehemu inayobaki
anaifanya kuwa mungu,
kuwa sanamu yake ya
kuchongwa.

Anaiinamia na kuiabudu.
Anasali kwake na kusema:
“Niokoe, kwa maana wewe
ni mungu wangu.”^e

18 Hawajui chochote, hawae-
lewi chochote,^f

Kwa sababu macho yao

44:13 *Au “madhabahu.”

yamefungwa kabisa na hayawezi kuona, Na moyo wao hauna ufa-hamu.

- 19** Hakuna mtu anayetafakari moyoni mwake Wala aliye na ujuzi na uelewaji, anayesema: “Nusu yake niliiteketeza motoni, Nami nimeoka mkate juu ya makaa yake na kuchoma nyama ya kula. Basi, je, ninapaswa kutumia sehemu inayobaki kutengeneza kitu kina-chochukiza?”^a

Je, ninapaswa kuabudu kipande cha mbao?”^{*}

- 20** Anakula majivu. Moyo wake mwenyewe uliodanganyika ume-mpotosha. Hawezi kujiokoa, ^{*} wala hasemi: “Je, hamna uwongo katika mkono wangu wa kulia?”
- 21** “Kumbuka mambo haya, Ee Yakobo, na wewe, Ee Israeli, Kwa maana wewe ni mtumishi wangu. Nilikutokeza, nawe ni mtumishi wangu.^b Ee Israeli, sitakusahau.^c

- 22** Nitayafuta kabisa makosa yako kama kwa wingu^d Na dhambi zako kama kwa wingu zito. Rudi kwangu, kwa maana nitakukomboa.^e

- 23** Pigeni vigelegele kwa shangwe, enyi mbingu, Kwa maana Yehova ametenda! Pazeni sauti kwa ushindi,

44:19 ^{*}Au “ubao uliokauka.” **44:20** ^{*}Au “kuokoa nafsi yake.”

SURA YA 44

a Kum 27:15

b Isa 43:1
Isa 44:1

c Isa 49:15

d Zb 51:1
Zb 103:12
Isa 1:18
Isa 43:25
Yer 33:8
Mdo 3:19

e Isa 1:27
Isa 48:20
Isa 59:20

Safu ya 2

a Isa 49:13
Isa 55:12

b Isa 60:21

c Isa 44:6

d Ayu 26:7
Isa 40:22

e Isa 42:5
Isa 48:13

f Ho 9:7

g 2Sa 15:31
Isa 29:14

h Yos 23:14
Isa 55:10, 11
Zek 1:6

i Zb 147:2

j Isa 60:10

k Isa 61:4

l Isa 42:15
Yer 50:38
Ufu 16:12

enyi sehemu zenye kina za dunia!

Pazeni sauti kwa shangwe, enyi milima,^a

Ewe msitu, na miti yako yote!

Kwa maana Yehova amekomboa Yakobo,

Na juu ya Israeli anaonyesha fahari yake.”^b

- 24** Yehova, Mkombozi wako,^c Aliyekuumba tangu ulipo-kuwa tumboni, anasema kivi:

“Mimi ni Yehova, niliyeu- mba kila kitu.

Nilizitandaza mbingu mimi mwenyewe,^d

Na kuitandaza dunia.^e

Ni nani aliyekuwa pamoja nami?

- 25** Ninazivuruga ishara za wale wanaoongea maneno matupu,^{*}

Na mimi ndiye ninayewafanya wabashiri watende kama wapumbavu;^f

Ninayewavuruga watu wenyekima

Na kubadili ujuzi wao kuwa upumbavu;^g

- 26** Ni mimi ninayefanya neno la mtumishi wangu litimie

Na kutimiza kikamili utabiri wa wajumbe wangu;^h

Ninayesema kuhusu Yerusalemu, ‘Litakaliwa,’ⁱ

Na kuhusu majiji ya Yuda, ‘Yatajengwa upya,’^j

Nami nitajenga upya magofu yake;^k

- 27** Ninayeviambia vilindi vya maji, ‘Kauka, Nami nitaikausha mito yako yote’;^l

- 28** Ninayesema kumhusu

44:25 ^{*}Au “manabii wa uwongo.”

Koreshi,^a ‘Yeye ni mchuingaji wangu,
Naye atatimiza kikamili mapenzi yangu yote’;^b
Ninayesema kuhusu Yerusalemu, ‘Litajengwa upya,’

Na kuhusu hekalu, ‘Msingi wako utawekwa.’^c

45 Hivi ndivyo Yehova anavyomwambia mtiwa-mafuta wake, Koreshi,^d

Ambaye nimeushika mko-
no wake wa kulia^e
Ili kuyatiisha mataifa mbele yake,^f
Kuwanyang’anya silaha* wafalme,
Kufungua mbele yake milango yenye pande mbili,
Hivi kwamba malango hayatafungwa:

2 “Mimi nitaenda mbele yako,^g

Nami nitavisawazisha vilima.

Nitaivunja milango ya shaba vipandevipande,
Nami nitayakata makomeo ya chuma.^h

3 Nitakupa hazina zilizo gizani

Na hazina zilizofichwa mafichoni,ⁱ

Ili ujue kwamba mimi ni Yehova,
Mungu wa Israeli, anayekuita kwa jina lako.^j

4 Kwa ajili ya mtumishi wangu Yakobo na Israeli niliyemchagua,
Ninakuita kwa jina.

Ninakupa jina la heshima, ingawa hukunijua.

5 Mimi ni Yehova, na hakuna mwingine yeyote.

45:1 *Tnn., “Kuvifungua viuno vya.”

SURA YA 44

a Ezz 1:1, 2
Isa 41:25
Isa 45:1
Isa 46:11
Da 10:1

b Isa 48:14

c 2Nya 36:22, 23
Ezz 6:3
Isa 45:13

SURA YA 45

d Ezz 1:1, 2
Isa 44:28

e Isa 45:4

f Isa 13:17
Isa 41:25

g Isa 13:4

h Zb 107:16

i Yer 50:35, 37

j Ezz 1:1, 2
Isa 44:28

Safu ya 2

a Kum 4:35, 39
Kum 32:39

b 1Sa 17:46
Zb 102:15, 16
Isa 37:20

c Zb 83:18

d Mwa 1:3
Yer 31:35

e Kut 10:21
Zb 104:20

f Isa 26:12

g Mhu 7:14
Amo 3:6

h Eze 34:26

i Isa 61:11

j Isa 29:16
Yer 18:6
Ro 9:20

Hakuna Mungu ila mimi.^a
Nitakuimarisha,* ingawa hukunijua,

6 Ili watu wajue

Kutoka mashariki hadi magharibi*
Kwamba hakuna mwingine ila mimi.^b

Mimi ni Yehova, na hakuna mwingine yeyote.^c

7 Ninatengeneza nuru^d na kuumba giza,^e
Ninatokeza amani^f na kuumba msiba;^g

Mimi, Yehova, ninafanya mambo hayo yote.

8 Enyi mbingu, leteni mvua kutoka juu;^h
Mawingu na yamwage uadilifu.

Dunia na ifunguke na kuzaa wokovu kwa wingi,
Na ichipushe uadilifu wakati uleule.ⁱ

Mimi, Yehova, nimeiumba.^j
9 Ole wake yule anayeshindana* na Muumba wake,[#]
Kwa maana yeye ni kigae cha udongo tu
Kati ya vigae vingine vya udongo vilivyo ardhini!

Je, udongo unapaswa kumuuliza Mfinyanzi:[^]
“Unatengeneza nini?”^j

Au kitu ulichokitengeneza kinapaswa kuuliza:
“Yeye hana mikono?”[®]

10 Ole wake anayemwambia baba: “Unazaa nini?”
Na kumwambia mwa-

45:5 *Tnn., “Nitakufunga kiuno kwa nguvu.” 45:6 *Au “Kutoka mawio hadi machweo.” 45:9 *Au “anayebishana.” #Au “na yule aliyemtengeneza.” ^Au “yule aliyeutengeneza.” ®Au labda, “Je, udongo unapaswa kusema: ‘Kazi yako haina vishikio?’”

namke: "Unajifungua nini?"*

- 11** Yehova, Mtakatifu wa Israeli na Muumba wake,^a anasema hivi: "Je, mnathubutu kuniuliza kuhusu mambo yanayokuja Na kuniamuru kuhusu wanangu^b na kuhusu kazi za mikono yangu?"
- 12** Niliiumba dunia^c na kumuumba mwanadamu juu yake.^d Nilizitandaza mbingu kwa mikono yangu mwenyewe,^e Nami ninaliamuru jeshi lake lote."^f
- 13** "Nimemwinua mtu katika uadilifu,^g Nami nitazinyoosha njia zake zote. Yeye ndiye atakayelijenga jiji langu^h Na kuwaweka huru bila bei au rushwaⁱ watu wangu waliotekwa,"^j asema Yehova wa majeshi.
- 14** Yehova anasema hivi: "Faida ya* Misri na bidhaa za* Ethiopia na Wasabea, watu warefu, Watakuja kwako na kuwa wako. Watatembea nyuma yako wakiwa na minyororo. Watakuja na kukuinamia.^k Watasali kwako wakisema, 'Kwa hakika Mungu yuko pamoja nawe,^l Na hakuna mwingine yeyote; hakuna Mungu mwingine.'"

45:10 *Au "Una uchungu wa kuzaa nini?" **45:14** *Au labda, "Wafanyakazi wa." #Au labda, "wafanyabiashara wa."

SURA YA 45

a Isa 43:3

b Ho 1:10

c Mwa 1:1
Isa 40:28

d Mwa 1:27

e Isa 44:24
Yer 32:17
Zek 12:1

f Ne 9:6

g Isa 42:6

h 2Nya 36:23
Ezr 1:2, 3
Isa 44:28i Isa 14:16, 17
Isa 43:14
Isa 49:25

j Isa 13:17

k Est 8:17
Isa 14:1, 2
Isa 49:23
Isa 60:14
Isa 61:5

l Zek 8:23

Safu ya 2

a Isa 43:11
Isa 60:16
Tit 1:3b Zb 97:7
Isa 44:9c Isa 26:4
Isa 51:6d Isa 29:22
Isa 54:4
Yoe 2:26
Sef 3:11e Isa 42:5
Yer 10:12f Zb 78:69
Zb 104:5
Zb 119:90
Met 3:19g Mwa 1:28
Mwa 9:1
Zb 37:29
Zb 115:16

h Isa 48:16

i Zb 111:7, 8
Zb 119:137j Isa 66:20
Yer 50:28

15 Kwa kweli wewe ni Mungu anayejificha, Ee Mungu wa Israeli, Mwo-kozi.^a

16 Wote wataaibishwa na kufedheheshwa; Watengenezaji wote wa sanamu wataenda zao kwa aibu.^b

17 Lakini Israeli ataokolewa na Yehova kwa wokovu wa milele.^c

Hamtaaibishwa wala kufedheheshwa kwa umilele wote.^d

18 Kwa maana Yehova, Muumba wa mbingu,^e Mungu wa kweli, Yule aliyeiumba dunia, Yule aliyeitengeneza na kuifanya imara kabisa,^f Ambaye hakuumba tu bila sababu,^g lakini aliiumba ili ikaliwe, anasema hivi:^g

"Mimi ni Yehova, wala hakuna mwingine.

19 Sikusema nikiwa mafichoni,^h katika nchi yenye giza; Sikuuambia uzao wa* Yakobo,

'Nitafuteni tu bila sababu.'^h

Mimi ni Yehova, ninayese- ma mambo ya uadilifu na kutangaza mambo manyoofu.ⁱ

20 Kusanyikeni pamoja mje. Karibieni pamoja, ninyi mlioponyoka kutoka kwa mataifa.^j Wale wanaobeba sanamu zilizocho ngwa hawajui chochote

45:18 *Au labda, "ili iwe tupu." **45:19** *Tnn., "Sikuiambia mbegu ya." #Au "Nitafuteni bure."

Na wanasali kwa mungu ambaye hawezi kuwa-
okoaa.^a

- 21** Toeni taarifa yenu, leteni kesi yenu.

Na washauriane pamoja kwa umoja.

Ni nani aliyetabiri jambo hili zamani za kale

Na kulitangaza tangu nyakati zilizopita?

Je, si mimi, Yehova?

Hakuna Mungu mwingine ila mimi;

Mungu mwadilifu na Mwo-
kozi,^b hakuna mwingine isipokuwa mimi.^c

- 22** Geukeni mje kwangu mwokolewe,^d miisho yote ya dunia,

Kwa maana mimi ni Mungu, na hakuna mwingine.^e

- 23** Nimeapa kwa nafsi yangu; Neno limetoka kinywani mwangu katika uadilifu, Nalo halitarudi.^f

Kila goti litapigwa mbele zangu,

Kila ulimi utaapa kuwa mshikamanifu^g

- 24** Na useme, 'Kwa hakika katika Yehova kuna uadilifu wa kweli na nguvu.

Wale wote wenye ghadhabu dhidi yake watakuja mbele zake kwa aibu.

- 25** Katika Yehova uzao* wote wa Israeli utathibitika kuwa sawa,^h

Nao watajigamba katika yeye."^h

- 46** Beli anainama chini,ⁱ Nebo anainama.

Sanamu zao zimewekwa juu ya wanyama, juu ya

SURA YA 45

a Isa 42:17
Yer 50:2

b Isa 43:3

c Kum 4:39
Isa 44:8
Mk 12:32

d Mik 7:7

e Kum 4:35

f Isa 55:10, 11

g Kum 6:13
Ro 14:11

h Isa 61:9

SURA YA 46

i Yer 50:2
Yer 51:44

Safu ya 2

a Isa 45:20

b Isa 1:9

c Kut 19:4
Kum 1:31
Isa 44:2

d Isa 41:4

e Isa 43:13

f Kut 15:11

g Mdo 17:29

h Isa 40:19
Yer 10:8, 9

i Isa 44:16, 17
Da 3:1, 5

j Yer 10:5

wanyama wanaobeba mizigo,^a

Kama mizigo inayowalemea wanyama waliochoka.

- 2** Wanainama na kujiinamisha pamoja;

Hawawezi kuiokoa mizigo,*

Nao wenyewe wanaenda utekwani.

- 3** "Nisikilize mimi, Ee nyumba ya Yakobo, nanyi nyote mnaobaki wa nyumba ya Israeli,^b

Ninyi niliowategemeza tangu mlipozaliwa na kuwabeba tangu tumboni.^c

- 4** Hata utakapozeeka nita-kuwa yuleyule;^d

Hata kichwa chako kikiwa na mvi nitaendelea kuku-beba.

Kama nilivyofanya, nita-kubeba na kukuchukua na kukuokoa.^e

- 5** Mtanifaninisha na nani au kunifanya niwe sawa na nani au kunilinganisha na nani,^f

Ili tufanane naye?^g

- 6** Kuna wale wanaomwaga dhahabu kwa wingi kuto-ka kwenye mikoba yao;

Wanapima fedha katika mizani.

Wanamwajiri mfua chuma, naye huitengeneza kuwa mungu.^h

Kisha wanasujudu, naam, wanaiabudu.^{*i}

- 7** Wanaiinua na kujitwika mabegani;^j

Wanaibeba na kuiweka mahali pake, nayo husi-mama papo hapo.

46:2 *Yaani, sanamu zilizobebwa na wanyama. 46:6 *Tnn., "wanaiinamia."

Haiondoki mahali pake.^a
Wanaipazia sauti, lakini
haiwajibu;

Haiwezi kumwoko a yeyote
kutoka katika taabu
yake.^b

8 Kumbukeni hilo, na mjipe
ujasiri.

Litieni moyoni, ninyi wa-
kosaji.

9 Kumbukeni mambo ya
kwanza* ya zamani za
kale,

Kwamba mimi ni Mungu,
na hakuna mwingine.

Mimi ni Mungu, na hakuna
aliye kama mimi.^c

10 Tangu mwanzo ninatabiri
matokeo,

Na tangu zamani za kale
mambo ambayo bado ha-
yajafanywa.^d

Ninasema, 'Uamuzi* wa-
ngu utasimama,^e

Nami nitafanya jambo lolo-
te ninalopenda.^f

11 Ninamwita kutoka masha-
riki^g ndege anayewinda,^g

Kutoka nchi ya mbali mtu
atakatetekeleza uamuzi*
wangu.^h

Nimesema, nami nitaliti-
miza.

Nimekusudia, nami pia ni-
talitekeleza.ⁱ

12 Nisikilizeni, ninyi mlio na
moyo mkaidi,*

Ninyi mlio mbali sana na
uadilifu.

13 Nimeuleta karibu uadilifu
wangu;

Hauko mbali sana,
Na wokovu wangu hauta-
kawia.^j

46:9 *Au "awali." **46:10, 11** *Au "ku-
sudi; shauri." **46:11** [#]Au "upande wa
mapambazuko ya jua." **46:12** *Tnn.,
"moyo wenye nguvu."

SURA YA 46

a Isa 5:3

b 1Fa 18:26
Isa 37:37, 38
Yon 1:5

c Kum 32:26

d Isa 42:9
Isa 45:21

e Zb 33:11

f Zb 135:6
Isa 55:10, 11

g Isa 41:2
Isa 45:1

h Ezz 1:1, 2
Isa 44:28
Isa 48:14

i Hes 23:19
Ayu 23:13

j Isa 12:2
Isa 51:5
Isa 62:11

Safu ya 2

a Isa 44:23
Isa 60:21

SURA YA 47

b Zb 137:8
Yer 50:41, 42

c Da 5:30

d Kum 32:35, 41
Zb 94:1

e Isa 41:14
Isa 43:3
Isa 44:6

f Isa 47:1

g Isa 13:19
Isa 14:4
Ufu 17:5

h 2Nya 36:15, 16
Isa 42:24, 25
Zek 1:15

i Kum 28:63
Eze 24:21

j Yer 52:14

k 2Fa 25:18-21
Zb 137:8

l Kum 28:49, 50

Nitaleta wokovu katika Sa-
yuni, na fahari yangu
kwa Israeli."^a

47 Shuka uje uketi mavu-
mbini,

Ewe binti ya Babiloni uliye
bikira.^b

Keti ardhini ambapo haku-
na kiti cha ufalme,^c

Ewe binti ya Wakaldayo,
Kwa maana watu hawa-
takuita tena wewe
mwororo na aliyede-
kezwa.

2 Chukua jiwe la kusagia na
usage unga.

Vua shela yako.

Vua rinda lako, funua mi-
guu yako.

Vuka mito.

3 Uchi wako utafunuliwa.

Aibu yako itaonekana.

Nitalipiza kisasi,^d na haku-
na mtu atakayenizua.*

4 "Yule anayetukombo a
—Yehova wa majeshi ndilo
jina lake—

Ndiye Mtakatifu wa
Israeli."^e

5 Keti hapo kimya na uingie
gizani,

Ewe binti ya Wakaldayo;^f

Hawatakuita tena Bi-
mkubwa* wa Falme.^g

6 Nilikuwa na ghadhabu ku-
waelekea watu wangu.^h

Niliutia unajisi urithi
wangu,ⁱ

Nami nikawatia mkononi
mwako.^j

Lakini hukuwaonyesha re-
hema.^k

Hata juu ya wazee uliweka
nira nzito.^l

47:3 *Au labda, "sitakutana na yeyote
kwa fadhili." **47:5** *Au "Malkia."

- 7** Ulisema: “Sikuzote nitakuwa Bimkubwa, * milele.”^a
Hukutia mambo haya moyoni mwako;
Hukufikiria mwisho wa jambo hilo.
- 8** Sasa sikia jambo hili, ewe mpenda raha,^b
Unayeketi kwa usalama, unayesema moyoni mwako:
“Mimi ndiye, na hakuna mwingine.”^c
Sitakuwa mjane.
Sitajua kamwe inavyokuwa kupoteza watoto.”^d
- 9** Lakini mambo haya majiwa yatacupata ghafla, kwa siku moja:^e
Kupoteza watoto na ujane. Yatacupata kwa kipimo kamili^f
Kwa sababu ya * ulozi wako mwingi na uchawi wako wenye nguvu.^g
- 10** Uliutumaini uovu wako. Ulisema: “Hakuna anayeniona.”
Hekima na ujuzi wako ndivyo vilivyokupotosha, Nawe unasema moyoni mwako: “Mimi ndiye, na hakuna mwingine.”
- 11** Lakini utapatwa na msiba, Na hakuna hirizi uka yoyote itakayouzuia.*
Utapatwa na shida; nawe hutaweza kuizuia.
Utakumbwa na uharibifu wa ghafla ambao huja-wahi kamwe kuona.^h
- 12** Basi, endelea kufanya uchawi na ulozi wako mwingi,ⁱ

47:7 *Au “Malkia.” 47:9 *Au labda, “Licha ya.” 47:11 *Au “Nawe hutajua jinsi ya kuuzuia kwa hirizi.”

SURA YA 47

a Da 4:30
Ufu 18:7

b Ufu 18:3

c Da 5:22, 23

d Ufu 18:7

e Ufu 18:10

f Yer 51:29

g Eze 21:21
Da 5:7
Ufu 18:23

h Ufu 18:10

i Da 2:2

Safu ya 2
a Da 5:7

b Yer 51:6

SURA YA 48

c Mwa 32:28

d Kum 6:13

Ambao umeutaabikia tangu ujana wako.

Labda utafaidika;
Labda utawatisha watu.

- 13** Umechoka kwa wingi wa washauri wako.

Na wasimame sasa na kukuokoa,

Wale wanaoabudu mbingu, * wanaotazama nyota,^a

Wale wanaotoa ujuzi wakiwa ti wa miezi mipya

Kuhusu mambo yatakayokupata.

- 14** Tazameni! Wao ni kama majani makavu.

Moto utawateketeza kabisa.

Hawawezi kujiokoa* kuto-ka kwenye nguvu za mwali wa moto.

Hawa si makaa ya kujipasha moto,

Na huu si moto wa kuota.

- 15** Ndivyo wachawi wako watakavyokuwa kwako,

Wale ambao ulitaabika naotangu ujana wako.

Watatanganga, kila mmoja kuelekea upande wake.*

Hakutakuwa na yeyote wa kukuokoa.^b

- 48** Sikieni hili, enyi watu wa nyumba ya Yakobo,

Ninyi mnaojiita kwa jina la Israeli^c

Na ambao mmetoka katika maji ya Yuda,*

Ninyi mnaoapa kwa jina la Yehova^d

47:13 *Au labda, “Wale wanaozigawa mbingu; Wanajimu.” 47:14 *Au “kuzio-koa nafsi zao.” 47:15 *Tnn., “kuelekea eneo lake.” 48:1 *Au labda, “mnaotoka Yuda.”

- Na mnaomwitia Mungu wa Israeli,
Ingawa si katika kweli na uadilifu.^a
- 2** Kwa maana wanajiita kwa jina la jiji takatifu^b
Na kutafuta msaada wa Mungu wa Israeli,^c
Ambaye jina lake ni Yehova wa majeshi.
- 3** “Mambo ya kwanza* niliwaambia zamani za kale.
Yalitoka kinywani mwangu,
Nami niliyatangaza.^d
Kwa ghafla nilichukua hatua, nayo yakatokea.^e
- 4** Kwa sababu nilijua jinsi ulivyo mkaidi
—Kwamba shingo yako ni kano ya chuma na paji la uso wako ni shaba^f—
- 5** Nilikuambia zamani za kale.
Kabla halijatukia, nilikufanya ulisikie,
Hivi kwamba hungeweza kufema, ‘Sanamu yangu ilifanya hivi;
Sanamu yangu ya kuchoingwa na sanamu yangu ya chuma* ziliamuru jambo hili.’
- 6** Umesikia na kuona mambo haya yote.
Je, hutayatangaza?^g
Kuanzia sasa na kuendelea ninakutangazia mambo mapya,^h
Siri zilizofichwa ambazo hujazijua.
- 7** Ni sasa yanapoumbwa, si zamani za kale,
Mambo ambayo kabla ya leo hukuwahi kuyasikia,
Hivi kwamba huwezi ku-

48:3 *Au “awali.” 48:5 *Au “sanamu yangu ya kuyeyushwa.”

SURA YA 48

a Luv 19:12
Sef 1:4, 5

b Isa 52:1

c Yer 21:1, 2

d Isa 42:9

e Yos 21:45
Isa 55:10, 11

f Kut 32:9
2Fa 17:13, 14
2Nya 36:15, 16
Zb 78:8
Eze 3:7

g Isa 43:10

h Isa 42:9
Isa 65:17

Safu ya 2

a Isa 29:10

b Yer 5:11
Yer 9:2

c Kum 9:7
Zb 95:10

d 1Sa 12:22
Zb 25:11
Zb 79:9
Yer 14:7

e Ne 9:30, 31
Zb 78:38

f Met 17:3

g Isa 1:25
Yer 9:7

h Isa 48:9

i Eze 20:9

j Isa 43:13
Isa 46:4

k Isa 44:6
Ufu 1:8
Ufu 22:13

l Ayu 38:4

m Isa 40:22
Isa 42:5

sema, “Tazama! Tayari ninayajua.”

- 8** Hapana, hujasikia,^a hujajua,
Na zamani masikio yako hayakuwa yamefunguliwa.
Kwa maana ninajua kwa-mba wewe ni mwenye hila sana,^b
Nawe umeitwa mkosaji tangu ulipozaliwa.^c
- 9** Lakini kwa sababu ya jina langu nitaizuia hasira yangu;^d
Kwa ajili ya sifa yangu mwenyewe nitajizua, Nami sitakuangamiza.^e
- 10** Tazama! Nimekusafisha, lakini si kama fedha.^f
Nimekujaribu* katika tanuru la kuyeyushia la mateso.^g
- 11** Nitatenda kwa ajili yangu mwenyewe, kwa ajili yangu mwenyewe nitatenda,^h
Ninawezaje kukubali nitiwe unajisi?ⁱ
Simpi yeyote utukufu wangu.*
- 12** Nisikilize mimi, Ee Yakobo, na Israeli, ambaye nimenwita.
Mimi ni yuleyule.^j Mimi ndiye wa kwanza; mimi pia ndiye wa mwisho.^k
- 13** Mkono wangu mwenyewe uliweka msingi wa dunia,^l
Na mkono wangu wa kueme ulizitandaza mbingu.^m
Ninapoziita, zinasimama pamoja.

48:10 *Au “Nimekuchunguza.” Au labda, “Nimekuchagua.” 48:11 *Au “Sishiriki utukufu wangu na yeyote.”

14 Kusanyikeni pamoja, ninyi nyote, msikilize.

Ni nani kati yao ameyatanga ngaza mambo haya?

Yehova amempenda.^a

Atatekeleza mapenzi yake dhidi ya Babiloni,^b

Na mkono wake utawashambulia Wakaldayo.^c

15 Mimi mwenyewe nimesema, nami nimemwita.^d

Nimemleta, na njia yake itafanikiwa.^e

16 Nikaribieni, msikie jambo hili.

Tangu mwanzoni kabisa sijasema kwa siri.^f

Tangu lilipotokea nilikuwapo.”

Na sasa Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amenituma, na* roho yake.

17 Yehova, Mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli,^g anasema hivi:

“Mimi, Yehova, ni Mungu wako,

Ninayekufundisha ili ujifaidi mwenyewe,^{*h}

Ninayekuongoza katika njia unayopaswa kute-mbea.ⁱ

18 Laiti ungesikiliza amri zangu!^j

Ndipo amani yako ingekuwa kama mto.^k

Na uadilifu wako kama mawimbi ya bahari.^l

19 Uzao wako ungekuwa mwingi* kama mchanga

Na wazao wako kama chembe zake.^m

Jina lao halingefutiliwa mbali kamwe wala kuangamizwa kutoka mbele zangu.”

SURA YA 48

a Isa 45:1

b Isa 44:28

c Isa 13:19
Yer 50:13

d Isa 41:2

e Isa 45:5

f Isa 45:19

g Isa 43:14
Isa 44:6
Isa 54:5

h 1Fa 8:36
Zb 25:8
Isa 54:13
Mik 4:2

i Zb 32:8
Isa 30:20, 21
Isa 49:10

j Kum 5:29
Zb 81:13, 14

k Zb 119:165
Isa 32:18
Isa 66:12

l Amo 5:23, 24

m Mwa 22:15, 17
Yer 33:22
Ho 1:10

Safu ya 2

a Yer 50:8
Ufu 18:4

b Isa 49:13

c Yer 50:2

d Yer 31:10, 11

e Kut 15:24, 25
Kum 8:14, 15
Isa 43:19

f Kut 17:5, 6
Hes 20:11

g Isa 57:20, 21

SURA YA 49

h Isa 55:4

i Isa 44:2
Isa 46:3

j Isa 51:16

k Isa 43:10

l Isa 44:23

20 Tokeni Babiloni!^a

Kimbieni kutoka kwa Wakaldayo!

Litangazeni kwa vigelegele vya shangwe! Litangazeni!^b

Lijulisheni mpaka kwenye miisho ya dunia.^c

Semeni: “Yehova amekomboa mtumishi wake Yakobo.^d

21 Hawakupata kiu alipowangoza katika maeneo yaliyoharibiwa.^e

Alifanya maji yatiririke kutoka kwenye mwamba kwa ajili yao;

Aliupasua mwamba maji yakabubujika.”^f

22 “Hakuna amani kwa wao-vu,”^g asema Yehova.

49 Nisikilizeni, enyi visiwa, Kazeni fikira, enyi mataifa yaliyo mbali.^h

Yehova aliniita kabla sijazaliwa.^{*i}

Tangu nilipokuwa katika tumbo la mama yangu amelitaja jina langu.

2 Alifikanya kinywa changu kuwa kama upanga mkali;

Amenificha katika kivuli cha mkono wake.^j

Alinifanya kuwa mshale uliosuguliwa;^{*k}

Alinisitiri katika podo lake.

3 Aliniambia: “Wewe ni mtumishi wangu, Ee Israeli,^k Ambaye kupitia kwake nitayonesha fahari yangu.”^l

4 Lakini nilisema: “Nimeji-taabisha bure.

49:1 * Tnn., “kutoka katika tumbo la uzazi.” **49:2** * Au “uliong’arishwa.”

48:16 *Au “pamoja na.” **48:17** *Au “kwa faida yako.” **48:19** *Tnn., “Mbegu yako ingekuwa nyingi.”

Nilitumia nguvu zangu
kwa ajili ya jambo lisilo
halisi, kwa ubatili.

Lakini kwa hakika hu-
kumu yangu iko na
Yehova,*

Na malipo yangu yako[#] na
Mungu wangu.”^a

- 5** Na sasa Yehova, Yule
aliyeniumba tangu tu-
mboni niwe mtumishi
wake,

Amesema kwamba nimru-
dishe Yakobo kwake,
Ili watu wa Israeli wakusa-
nyike kwake.^b

Nitatukuzwa machoni pa
Yehova,

Na Mungu wangu tayari
atakuwa nguvu zangu.

- 6** Naye akasema: “Haitoshi
tu wewe kuwa mtumishi
wangu

Ili kuyainua makabila ya
Yakobo

Na kuwarudisha wale wa-
lihifadhiwa wa Israeli.

Nimekutoa pia ili uwe nuru
ya mataifa,^c

Ili wokovu wangu ufike
kwenye miisho ya du-
nia.”^d

7 Yehova, Mkombozi wa
Israeli, Mtakatifu wake,^e ana-
mwambia hivi yule anaye-
dharauliwa,^f yule anayechuki-
wa na taifa, mtumishi wa wa-
tawala:

“Wafalme wataona na ku-
simama,

Na wakuu watainama chini
Kwa sababu ya Yehova,
ambaye ni mwaminifu,^g

Mtakatifu wa Israeli,
ambaye amekuchagua.”^h

49:4 *Au “Yehova atanitendea kwa haki.” #Au “thawabu yangu iko.”

SURA YA 49

a Isa 40:10

b Isa 56:8

c Isa 42:6
Mt 12:18
Lu 2:30, 32d Zb 98:2
Isa 11:10
Isa 52:10
Mdo 13:47

e Isa 43:14

f Isa 53:3

g Kum 7:9

h Isa 42:1

Safu ya 2

a Zb 69:13

b Lu 1:69
Lu 22:43
2Ko 6:2
Ebr 5:7

c Isa 42:6, 7

d Isa 54:3

e Zb 102:19, 20

f Zb 112:4
Isa 9:2
Lu 1:68, 79g Isa 55:1
Isa 65:13

h Isa 32:2

i Eze 34:23

j Zb 23:1, 2
Yer 31:9
Ufu 7:16, 17k Zb 107:6, 7
Isa 11:16
Isa 40:3, 4

l Kum 30:4

m Isa 43:5, 6

n Isa 42:10

o Isa 55:12

- 8** Yehova anasema hivi:
“Wakati wa kibali* niliku-
jibu,^a

Na katika siku ya wokovu
nilikusaidia;^b

Niliendelea kukulinda ili
nikutoe uwe agano kwa
ajili ya watu,^c

Ili kuitengeneza upya nchi,
Ili kuwafanya wamiliki uri-
thi wao ulio ukiwa,^d

- 9** Ili kuwaambia wafungwa,
“Tokeni nje!”^e

Na wale walio gizani,^f “To-
keni nje mwonekane!”
Watalisha kando ya bara-
bara,

Malisho yao yatakuwa
kando ya njia zilizoka-
nyagwa.*

- 10** Hawatakuwa na njaa, wala
hawatakuwa na kiu,^g

Wala joto kali wala jua ha-
litawachoma.^h

Kwa maana Yule ana-
yewaonyesha rehema
atawaongoza,ⁱ

Naye atawaongoza kando
ya chemchemi za maji.^j

- 11** Nitaifanya milima yangu
yote kuwa barabara,
Na barabara zangu kuu zi-
tainuliwa.^k

- 12** Tazameni! Hawa wanaku-
ja kutoka mbali sana,^l
Na tazameni! hawa wana-
toka kaskazini na kutoka
magharibi,

Na hawa kutoka nchi ya Si-
nimu.”^m

- 13** Pigeni vigelegele vya sha-
ngwe, enyi mbingu, na
ushangilie, Ee dunia.ⁿ

Milima na ichangamke
kwa kilio cha shangwe.^o

49:8 *Au “nia njema.” 49:9 *Au labda,
“vilima visivyo na kitu.”

- Kwa maana Yehova ame-wafariji watu wake.^a
Naye huwaonyesha rehema watu wake mwenyewe wanaoteseka.^b
- 14** Lakini Sayuni aliendelea kusema:
“Yehova ameniacha,^c na Yehova amenisahau.”^d
- 15** Je, mwanamke anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya
Au asimhurumie mwana wa tumbo lake?
Hata wanawake hawa wakisahau, mimi siwezi kamwe kukusahau.^e
- 16** Tazama! Nimekuchonga kwenye viganja vyangu. Kuta zako ziko mbele zangu daima.
- 17** Wana wako wanarudi haraka.
Wale waliokubomoa na kukuharibu wataondoka kwako.
- 18** Inua macho yako utazame pande zote.
Wote wanakusanyika pamoja.^f
Wanakuja kwako.
“Kwa hakika kama ninavyoishi,” asema Yehova,
“Utajivika hao wote kana kwamba ni mapambo,
Nawe utajifunga watu hao kama bibi harusi anavyofanya.
- 19** Ingawa maeneo yako yaliharibiwa na kuwa ukiwa na nchi yako ikawa magofu,^g
Sasa itakuwa ndogo sana kwa wale wanaokaa humo,^h
Na wale waliokumezaⁱ watakuwa mbali sana.^j

SURA YA 49

a Isa 12:1
Isa 40:1
Isa 66:13

b Isa 44:23
Isa 61:3
Yer 31:13

c Isa 54:7

d Omb 5:20

e Isa 44:21
Yer 31:20

f Isa 43:5, 6
Isa 60:4

g Isa 51:3

h Yer 30:18, 19

i Yer 51:34

j Yer 30:16

Safu ya 2

a Isa 54:1, 2

b Isa 43:5
Yer 31:17

c Omb 1:1

d Isa 62:4

e Ezr 1:3
Isa 11:10, 12
Isa 62:10

f Isa 60:4
Isa 66:20

g Isa 60:10, 16

h Isa 60:14

i Mik 7:16, 17

j Isa 25:9

20 Wana waliozaliwa ulipokuwa umefiwa watasema hivi ukisikia,
‘Mahali hapa ni padogo sana kwangu.

Nipeni nafasi zaidi hapa nikae.’^a

21 Nawe utasema moyoni mwako,
‘Ni baba gani aliyenizalia watoto hawa,

Kwa kuwa mimi ni mwanamke niliyefiwa na watoto, nami ni tasa,
Nami nilipelekwa uhamishoni na kufungwa?

Ni nani aliyewalea hawa?^b

Tazameni! Nilibaki peke yangu,^c

Sasa hawa wametoka wapi?”^d

22 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Tazameni! Nitayainulia mataifa mkono wangu,

Nami nitawainulia watu ishara yangu.”^e

Watawaleta wana wako wakiwa wamewabeba mikononi mwao^f

Na kuwabeba mabinti wako kwenye mabega yao.^f

23 Wafalme watakuwa watunzaji wako,^g

Na mabinti wao wa kifalme watakuwa walezi wako.

Watakuinamia kifudufudi^h

Na kuyaramba mavumbi ya miguu yako,ⁱ

Nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova;

Wale wanaonitumaini hawataaibika.”^j

49:22 *Au “nguzo yangu ya ishara.”
Tnn., “kifuani.”

24 Je, wale waliotekwa waweza kuchukuliwa kutoka kwa mtu mwenye nguvu,

Au, je, mateka wa mtu mkatili wanaweza kuo-
kolewa?

25 Lakini Yehova anasema hivi:

“Hata mateka wa mtu mwenye nguvu watachukuliwa,^a

Na wale waliotekwa na mtu mkatili wataokolewa.^b

Nitawapinga wale wanaokupinga,^c

Nami nitawaokoa wanao wako mwenyewe.

26 Nitawafanya wale wanaokutesa wale nyama yao wenyewe,

Nao watalewa kwa damu yao wenyewe kana kwamba ni kwa divai tamu.

Na watu wote* watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova,^d

Mwokozi wako^e na Mko-mbozi wako,^f

Mwenye Nguvu wa Yakobo.”^g

50 Yehova anasema hivi: “Kiko wapi cheti cha talaka^h cha mama yenu, ambaye nilimfukuza?

Au niliwauza kwa yupi kati ya wakopeshaji wangu?

Tazameni! Mliuzwa kwa sababu ya uovu wenu,ⁱ

Na mama yenu alifukuzwa kwa sababu ya makosa yenu wenyewe.^j

2 Basi, kwa nini nilipokuja, hapakuwa na mtu yeyote mahali hapa?

SURA YA 49

a Yer 29:14
Yer 46:27
Ho 6:11
Yoe 3:1

b Isa 52:2
Yer 29:10
Yer 50:34
Zek 9:11

c Isa 54:17

d Eze 39:28

e 1Ti 1:1

f Isa 41:14
Isa 48:20

g Isa 60:16

SURA YA 50

h Kum 24:1

i 2Fa 17:16, 17

j Isa 59:2
Yer 3:1

Safu ya 2

a Yer 35:15

b Isa 40:28
Isa 59:1

c Kut 14:21, 29
Zb 106:9
Isa 51:10

d Zb 107:33
Zb 114:1, 3
Isa 42:15
Nah 1:4

e Kut 10:21

f Kut 4:11
Yer 1:9

g Yoh 7:15, 46

h Mt 13:54

i Zb 40:6-8

j Mt 26:39
Flp 2:8

Kwa nini hakuna aliyejibu nilipoita?^a

Je, mkono wangu ni mfupi usiweze kukomboa,

Au je, sina nguvu za kuo-
koa?^b

Tazameni! Mimi huikausha bahari kwa kemeo langu;^c

Ninaifanya mito kuwa jangwa.^d

Samaki waliomo huoza kwa kukosa maji,

Nao hufa kwa sababu ya kiu.

3 Mimi hulivisha mbingu giza,^e

Nami huzifunika kwa nguo za magunia.”

4 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amenipa ulimi wa waliofundishwa,^{*f}

Ili nijue jinsi ya kumjibu[#] aliyechoka kwa neno linalofaa.^{△g}

Yeye huniamsha asubuhi baada ya asubuhi;

Huliamsha sikio langu ili lisikilize kama wale waliofundishwa.^h

5 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amelifungua sikio langu,

Nami sikuwa mwasi.ⁱ

Sikugeuka upande ulio kinyume.^j

6 Niliwapa mgongo wangu wale waliokuwa wakini-piga

Na mashavu yangu wale waliozing’oa ndevu zangu.

Sikuuficha uso wangu kutoka kwa mambo yenye

50:4 *Au “ulimi uliozoezwa vizuri.”

[#]Au labda, “kumwimarisha.” [△]Tnn., “kwa neno.”

kufedhehesha na kutoka kwa mate.^a

- 7 Lakini Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atani-saidia.^b

Ndiyo sababu sitafedheheka.

Ndiyo sababu nimeufanya uso wangu uwe kama jiwe gumu.^c

Nami ninajua kwamba sitaaibika.

- 8 Yule anayenitangaza kuwa mwadilifu yu karibu.

Ni nani anayeweza kuni-shtaki?^{*d}

Na tusimame pamoja.[#]

Ni nani aliyene na kesi dhidi yangu?

Na anikaribie.

- 9 Tazameni! Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atani-saidia.

Ni nani atakayenitangaza kuwa na hatia?

Tazameni! Wote watachakaa kama vazi.

Nondo* atawala.

- 10 Ni nani kati yenu anayemwogopa Yehova

Na kusikiliza sauti ya mtumishi wake?^e

Ambaye ametembea katika giza zito, bila mwangaza wowote?

Na alitumaini jina la Yehova na kujitegemeza juu ya* Mungu wake.

- 11 "Tazameni! Ninyi nyote mnaowasha moto, Mnaorusha cheche, Tembeeni katika nuru ya moto wenu,

50:8 *Au "kushindana nami?" #Au "tutazamane." 50:9 *Aina fulani ya mdudu mharibifu. 50:10 *Au "kumtegemea."

SURA YA 50

a Mt 26:67
Mk 14:65
Lu 22:63
Yoh 18:22

b Isa 49:8

c Eze 3:8, 9

d Ro 8:33

e Isa 42:1
Isa 53:11

Safu ya 2

SURA YA 51

a Mwa 21:2

b Mwa 12:1
Mwa 15:2

c 1Fa 4:20

d Zb 102:13
Isa 66:13
Yer 31:12

e Isa 44:26
Isa 61:4

f Mwa 2:8

g Isa 35:1
Isa 41:18

h Yer 33:10, 11

i Kut 19:6
Kum 7:6

j Isa 2:3
Mik 4:2

k Met 6:23

Kati ya cheche ambazo mmewasha.

Hili ndilo mtakalopata kutoka mkononi mwangu: Mtalala kwa maumivu makali.

- 51** "Nisikilizeni mimi, ninyi mnaofuatia uadilifu, Ninyi mnaomtafuta Yehova.

Uangalieni mwamba ambao mlichongwa kutoka kwake

Na machimbo ambamo mlichimbwa kutoka ndani yake.

- 2 Mwangalieni Abrahamu baba yenu

Na Sara^a aliyewazaa.*

Kwa maana Abrahamu alikuwa mmoja tu nilipomwita,^b

Nami nilimbariki na kumfanya kuwa wengi.^c

- 3 Kwa maana Yehova atali-fariji Sayuni.^d

Ataleta faraja kwa magofu yake yote,^e

Naye ataifanya nyika yake kuwa kama Edeni^f

Na jangwa lake tambarare kama bustani ya Yehova.^g

Kutakuwa na furaha na shangwe ndani yake, Kutoa shukrani na nyimbo tamu.^h

- 4 Nisikilizeni, enyi watu wangu,

Na mnitegee sikio, taifa langu.ⁱ

Kwa maana sheria itatoka kwangu,^j

Nami nitaifanya haki yangu kuwa nuru kwa watu.^k

51:2 *Au "aliyewazaa kwa uchungu wa kuzaa."

- 5** Uadilifu wangu unakaribia.^a
Wokovu wangu utatoka,^b
Na mikono yangu itayahukumu mataifa.^c
Visiwa vitanitumaini mimi,^d
Navyo vitaungojea mkono wangu.*
- 6** Inueni macho yenu mbinguni,
Na mtazame chini duniani.
Kwa maana mbingu zitatawanyika vipandevipande kama moshi;
Nayo dunia itachakaa kama vazi,
Na wakaaji wake watakufa kama mbu.*
Lakini wokovu wangu utadumu milele,^e
Na uadilifu wangu hautashindwa kamwe.^{#f}
- 7** Nisikilizeni mimi, ninyi mnaoujua uadilifu,
Watu walio na sheria* yangu moyoni mwao.^g
Msiogope dhahaka za wanadamu wanaoweza kufa,
Na msiogopeshe na matusi yao.
- 8** Kwa maana nondo atawala kabisa kama vazi;
Nondo* alaye nguo atawala kabisa kama sufu.^h
Lakini uadilifu wangu utadumu milele,
Na wokovu wangu kwa vizazi vyote."ⁱ
- 9** Amka! Amka! Jivike nguvu,
Ee mkono wa Yehova!

51:5 *Au "vitangojea nguvu zangu."
51:6 *Aina ya mbu anayelitwa *hak-kin-nam'* katika Kiebrania. #Au "hautavunjwa." 51:7 *Au "mafundisho." 51:8 *Au labda, "Mnyoo."

SURA YA 51

a Isa 46:13

b Isa 12:2
Isa 56:1c 1Sa 2:10
Isa 2:4

d Isa 60:9

e Isa 45:17

f Zb 102:25-27
Mt 24:35

g Yer 31:33

h Isa 50:9

i Isa 45:17
Lu 1:50

j Lu 1:51

Safu ya 2

a Zb 87:4
Zb 89:10
Isa 30:7b Kut 15:4
Ne 9:10, 11
Zb 106:22
Eze 29:3

c Kut 14:21, 22

d Zb 106:9

e Yer 31:11
Zek 10:10

f Isa 35:10

g Isa 61:7

h Isa 25:8
Isa 65:18, 19i Isa 49:13
Isa 66:13j Zb 118:6
Da 3:16, 17
Mt 10:28

k Isa 44:2

l Isa 40:22

Amka kama katika siku za zamani za kale, kama katika vizazi vilivyopita.

Je, si wewe uliyemvunja Rahabu*^a vipandevipande,

Uliyemchoma kwa silaha yule mnyama mkubwa sana wa baharini?^b

10 Je, si wewe uliyeikausha bahari, maji ya kilindi kikubwa?^c

Uliyevifanya vilindi vya bahari kuwa njia ili watu waliokombolewa wawuke?^d

11 Watu wa Yehova waliokombolewa watarudi.^e

Watakuja Sayuni kwa vigelegele vya shangwe,^f

Na shangwe isiyokoma itakuwa taji lao.*^g

Watakuwa na furaha na shangwe.

Huzuni na kilio cha uchungu vitakimbia.^h

12 "Mimi mwenyewe Ndiye ninayewafaraji."ⁱ

Kwa nini umwogope wanadamu anayeweza kufa ambaye atakufa/

Na mwana wa binadamu atakayenyauka kama majani mabichi?

13 Kwa nini unamsahau Yehova Muumba wako,^k
Yule aliyezetandaza mbingu/ na kuweka msingi wa dunia?

Mchana kutwa uliendelea kuhofu ghadhabu ya mkandamizaji,*

Kana kwamba angeweza kukuangamiza.

51:9 *Angalia Kamusi, uku. 2012.
51:11 *Tnn., "juu ya vichwa vyao."
51:13 *Au "yule anayekubana."

- Iko wapi sasa ghadhabu ya mkandamizaji?
- 14** Yule aliyejikunja katika minyororo atawekwa huru hivi karibuni;^a Hatakufa na kuingia shimoni, Wala hatakosa mkate.
- 15** Lakini mimi ni Yehova Mungu wako, Ninayeitibua bahari na kuvavuruga mawimbi yake^b —Yehova wa majeshi ndilo jina lake.^c
- 16** Nitayaweka maneno yangu katika kinywa chako, Nami nitakufunika kwa kuvuli cha mkono wangu,^d Ili kuzipanda mbingu na kuuweka msingi wa dunia^e Na kuwambia watu wa Sayuni, ‘Ninyi ni watu wangu.’^f
- 17** Amka! Amka! Simama, Ee Yerusalemu,^g Wewe ambaye umekunywa kutoka mkononi mwa Yehova kikombe chake cha ghadhabu. Umekunywa bilauri; Umemaliza kabisa kikombe kinachofanya watu wapepesuke.^h
- 18** Kati ya wana wote aliowazaa hakuna hata mmoja aliye hapo ili kumwongoza, Na kati ya wana wote aliowalea hakuna hata mmoja ambaye anamshika mkono.
- 19** Mambo hayo mawili yamekupata. Ni nani atakayekusikitikia? Maangamizi na uharibifu, njaa na upanga!ⁱ Ni nani atakayekufariji?!

SURA YA 51

a Ezz 1:2, 3
Isa 48:20
Isa 52:2

b Yer 31:35, 36
Yon 1:4

c Isa 47:4

d Kum 33:27
Zb 91:1

e Isa 65:17
Isa 66:8, 22

f Isa 60:14
Yer 31:33
Zek 8:8

g Isa 52:1
Isa 60:1

h Yer 25:15

i Eze 14:21

j Omb 1:17

Safu ya 2

a Omb 2:11

b Isa 51:17

c Isa 54:9
Isa 62:8

d Isa 49:25

SURA YA 52

e Hag 2:4

f Isa 51:17

g Isa 61:3

h Isa 35:8
Isa 60:21
Ufu 21:27

i Isa 51:14
Isa 61:1

- 20** Wana wako wamezimia.^a Wanalala chini katika kila pembe ya barabara Kama kondoo mwitu katika wavu. Wamejaa ghadhabu ya Yehova, kemeo la Mungu wako.”
- 21** Kwa hiyo tafadhali sikiliza jambo hili, Ewe mwanamke uliyeteseka na kulewa, lakini si kwa divai.
- 22** Bwana wako Yehova, Mungu wako anayewatetea watu wake anasema hivi: “Tazama! Nitakichukua kutoka mkononi mwako kile kikombe kinachofanya watu wapepesuke,^b Ile bilauri, kikombe changu cha ghadhabu; Hutakinywa tena.^c
- 23** Nitakitia mkononi mwa wale wanaokutesa,^d Wale waliokuambia, ‘Ina-ma chini ili tutembe juu yako!’ Basi ukaufanya mgongo wako kama ardhi, Kama barabara yao ya kutembea juu yake.”
- 52** Amka! Amka! Jivike nguvu,^e ewe Sayuni!^f Vaa mavazi yako maridadi,^g ewe Yerusalemu, jiji takatifu! Kwa maana mtu ambaye hajatahiriwa na mtu asiye safi hawataingia ndani yako tena.^h
- 2** Yakung’ute mavumbi, inuka na uketi, ewe Yerusalemu. Fungua pingu zilizo shingoni mwako, ewe binti ya Sayuni uliye mateka.ⁱ

3 Kwa maana Yehova anasema hivi:

“Ninyi mliuzwa bila malipo,^a

Na mtakombolewa bila pesa.”^b

4 Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Mwanzoni watu wangu walishuka kwenda Misri ili waishi huko wakiwa wageni;^c

Kisha Ashuru ikawakandamiza bila sababu.”

5 “Basi nifanye nini hapa?” auliza Yehova.

“Kwa maana watu wangu walichukuliwa bila malipo.

Wale wanaowatawala wanaendelea kupiga mayowe ya ushindi,”^d asema Yehova,

“Na daima, mchana kutwa, jina langu linavunjiwa heshima.”^e

6 Kwa sababu hiyo watu wangu watalijua jina langu;^f

Kwa sababu hiyo watajua siku hiyo kwamba mimi Ndiye ninayesema.

Tazama, ni mimi!”

7 Jinsi inavyopendeza juu ya milima, miguu ya yule anayeleta habari njema,^g

Anayetangaza amani,^h

Anayeleta habari njema za jambo bora,

Anayetangaza wokovu,

Anayeambia Sayuni: “Mungu wako amekuwa Mfalme!”ⁱ

8 Sikiliza! Walinzi wako wanapaza sauti.

Wanapiga vigelegele kwa shangwe pamoja,

SURA YA 52

a Isa 50:1

b Isa 45:13

c Mwa 46:5-7

d Zb 137:3

Yer 50:17

e Zb 74:10

Ro 2:24

f Eze 20:44

g Isa 40:9

Nah 1:15

Mdo 8:4

Ro 10:15

Efe 6:14, 15

h Lu 2:14

Mdo 10:36

Efe 2:17

i Zb 93:1

Isa 33:22

Mik 4:7

Mt 24:14

Ufu 11:15, 17

Safu ya 2

a Isa 61:4

b Isa 66:13

c Isa 44:23

d Isa 51:9

e Zb 22:27

Isa 49:6

f Isa 48:20

Yer 50:8

Yer 51:6

Zek 2:6

g Law 5:2

Eze 44:23

h 2Ko 6:17

Ufu 18:4

i Law 10:3

Hes 3:6, 8

Ezr 1:7

Ezr 8:30

j Kut 13:21

1Nya 14:15

k Isa 58:8

l Isa 42:1

Isa 61:1

Flp 2:5-7

m Zb 2:6

Zb 110:1

Isa 9:6

Mt 28:18

Kwa maana wataona waziwazi* Yehova atakapokusanya Sayuni tena.

9 Changamkeni, pigeni pamoja vigelegele kwa shangwe, enyi magofu ya Yerusalem,^a

Kwa maana Yehova amewafariji watu wake;^b amekomboa Yerusalem.^c

10 Yehova ameufunua wazi mkono wake mtakatifu mbele ya macho ya mataifa yote;^d

Miisho yote ya dunia itayaona matendo ya wokovu ya* Mungu wetu.^e

11 Ondokeni, ondokeni, tokeni humo,^f msiguse kitu chochote kichafu!^g

Tokeni kati yake,^h iweni safi,

Ninyi mnaobeba vyombo vya Yehova.ⁱ

12 Kwa maana hamtaondoka kwa wasiwasi,

Wala hamtahitaji kukiambia,

Kwa maana Yehova atawatangulia,^j

Na Mungu wa Israeli atakuwa mlinzi nyuma yenu.^k

13 Tazameni! Mtumishi wangu' atatenda kwa ufahamu.

Atainuliwa juu,

Atainuliwa na kukwezwa sana.^m

14 Kama alivyotazamwa na wengi kwa mshangao

—Kwa maana sura yake ilikuwa imeharibiwa kuliko ya mwanadamu mwingine yeyote

52:8 *Au “jicho kwa jicho.” 52:10 *Au “itaona ushindi wa.”

Na umbo lake lenye fahari
kuliko la binadamu—

15 Ndivyo atakavyoyashtua
mataifa mengi.^a

Wafalme watafunga vi-
nywa vyao* mbele yake,^b

Kwa sababu wataona
mambo ambayo hawa-
kuwa wameambiwa

Na kufikiria mambo
ambayo hawakuwa
wamesikia.^c

53 Ni nani ambaye amea-
mini jambo alilosikia
kutoka kwetu?*^d

Na mkono wa Yehova,^e
umefunuliwa kwa nani?*

2 Atapanda kama tawi^g
mbele yake,* kama mzizi
kutoka katika nchi iliyo-
kauka.

Hana umbo la kifahari,
wala utukufu wowote;^h

Na tunapomwona, sura
yake haituvutii.[#]

3 Alidharauliwa na kuepu-
kwa na wanadamu,ⁱ

Mtu aliyekusudiwa ku-
pata* maumivu na
aliyezoea magonjwa.

Ilikuwa kana kwamba uso
wake ulifichwa kutoka
kwetu.[#]

Alidharauliwa, nasi tuli-
mwona kuwa asiye na
maana.^j

4 Kwa kweli yeye mwenyewe
aliyabeba magonjwa
yetu,^k

52:15 *Au "hawatakuwa na la kusema."

53:1 *Au labda, "jambo ambalo tulisi-
kia?" 53:2 *Maneno "mbele yake" hue-
nda yanarejelea mtazamaji yeyote au
Mungu. *Au "hana sura ya pekee hivi
kwamba tumtamani." 53:3 *Au "ali-
yeelewa." *Au labda, "Alikuwa kama
mtu ambaye watu waligeuza mbali nyu-
so zao ili wasimtazame."

SURA YA 52

a Zb 2:2

b Zb 2:10
Zb 72:11

c Ro 15:20, 21

SURA YA 53

d Ro 10:16

e Isa 51:9

f Isa 40:5
Yoh 12:37, 38

g Isa 11:1
Zek 6:12

h Isa 52:14
Yoh 1:10
Flp 2:7

i Zb 22:7
Mt 26:67, 68
Yoh 6:66
1Pe 2:4

j Zek 11:13
Yoh 18:39, 40
Mdo 3:13, 14
Mdo 4:11

k Mt 8:14-17

Safu ya 2

a Law 16:21, 22
1Pe 2:24
1Yo 2:1, 2

b Zek 12:10
Yoh 19:34

c Da 9:24
Ro 4:25

d Mt 20:28
Ro 5:6, 19

e Kol 1:19, 20

f 1Pe 2:24

g 1Pe 2:25

h 1Pe 3:18

i Zb 22:12
Zb 69:4

j 1Pe 2:23

k Yoh 1:29
1Ko 5:7

l Mt 27:12-14
Mdo 8:32, 33

m Da 9:26
Mt 27:50

n Zek 13:7
Yoh 11:49, 50

o Ro 5:6
Ebr 9:26

o Mt 27:38

Na kujitwika maumivu
yetu.^a

Lakini tulimwona kama
mtu aliyepata mapigo,
aliyepigwa na Mungu na
kuteswa.

5 Lakini alichomwa*^b kwa
sababu ya makosa yetu;^c

Alipondwa kwa sababu ya
dhambi zetu.^d

Aliibeba adhabu ili tupate
amani,^e

Na kwa sababu ya majera-
ha yake tuliponywa.^f

6 Sisi sote tumetangatanga
kama kondoo,^g

Kila mmoja ameifuata njia
yake mwenyewe,

Na Yehova amefanya dha-
mbi yetu sote ikutane
naye.^h

7 Alikandamizwaⁱ na aliku-
bali kuteswa,^j

Lakini hakuthubutu kufu-
ngua kinywa chake.

Aliletwa kama kondoo ma-
chinjioni,^k

Kama kondoo jike aliye
kimya mbele ya wanao-
mkata manyoya,

Na hakuthubutu kufungua
kinywa chake.^l

8 Kwa sababu ya kizuizi* na
hukumu alichukuliwa;

Na ni nani atakayejishu-
ghulisha na habari za
kizazi chake?*

Kwa maana aliondolewa
katika nchi ya walio hai;^m

Alipata pigoⁿ kwa sababu
ya makosa ya watu wa-
ngu.ⁿ

9 Naye alipewa kaburi* pa-
moja na waovu,^o

53:5 *Au "alichomwa kwa silaha." 53:8
*Au "ukandamizaji." *Au "njia yake
ya maisha." *Au "Aliuawa." 53:9 *Au
"Na mtu ataoa kaburi lake."

Na pamoja na matajiri* ka-
tika kifo chake,^a

Ingawa hakuwa amefanya
kosa[#]

Na hakukuwa na udanga-
nyifu kinywani mwake.^b

10 Lakini yalikuwa mapenzi
ya Yehova* kumponda,
naye aliruhusu awe mgo-
njwa.

Ukitoa uhai wake[#] uwe
dhabihu ya hatia,^c

Ataona uzao wake,[^] atao-
ngeza siku zake,^d

Na kupitia kwake ma-
penzi[®] ya Yehova
yatafanikiwa.^e

11 Kwa sababu ya mateso*
yake, ataona na kuri-
dhika.

Kupitia ujuzi wake,
yule mwadilifu, mtumi-
shi wangu,^f

Atawaletea watu wengi
msimamo wa uadilifu,^g

12 Kwa sababu hiyo nitampa
fungu kati ya wengi,

Naye atagawa nyara pamo-
ja na wenye nguvu,
Kwa sababu aliumwaga
uhai wake* mpaka kifoⁱ

Naye alihesabiwa miongo-
ni mwa wakosaji;^j
Aliibeba dhambi ya watu
wengi,^k

Naye aliwatetea wakosaji.^l

54 "Piga vigelegele kwa
shangwe, wewe mwa-
namke tasa ambaye
hujazaa!^m

53:9 *Tnn., "mtu tajiri." #Au "ukatili."
53:10 *Au "Yehova alifurahia." #Au
"nafsi yake." ^Tnn., "Ataiona mbegu
yake." ®Au "mapendezi." 53:11 *Au
"maumivu ya nafsi." 53:12 *Au "alii-
mwaga nafsi yake."

SURA YA 53

a Mt 27:57-60
Mk 15:46
Yoh 19:41

b 1Pe 2:22

c Law 16:11
2Ko 5:21
Ebr 7:27

d Isa 9:7
1Ti 6:16

e Kol 1:19, 20

f Isa 42:1

g Ro 5:18, 19

h 1Pe 2:24

i Zb 22:14
Mt 26:27, 28
Ebr 2:14

j Mk 15:27
Lu 22:37
Lu 23:32, 33

k Mt 20:28
1Ti 2:5, 6
Tit 2:13, 14
Ebr 9:28

l Ro 8:34
Ebr 7:25
Ebr 9:26
1Yo 2:1, 2

SURA YA 54

m Isa 62:4

Safu ya 2

a Isa 44:23
Isa 49:13

b Isa 66:7, 8

c Gal 4:26, 27

d Isa 49:20

e Isa 33:20

f Isa 49:8
Eze 36:35

g Isa 41:10

h Isa 61:7

i Isa 44:2

j Eze 16:8
Ho 2:16

k Isa 44:6

l Zek 14:9
Ro 3:29

m Isa 49:14
Isa 62:4

Changamka na upaze sau-
ti kwa shangwe,^a wewe
ambaye hukuwahi kupa-
ta uchungu wa kuzaa,^b

Kwa maana wana* wa aliye
ukiwa ni wengi

Kuliko wana wa mwana-
mke aliye na mume,^{#c}
asema Yehova.

2 "Pafanye mahali pa hema
lako pawe na nafasi ku-
bwa zaidi.^d

Vitandaze vitambaa vya
hema lako tukufu la
ibada.

Usizuie, refusha kamba za
hema lako,

Na uviimarisha vingi vya
hema lako.^e

3 Kwa maana utaenea kulia
na kushoto.

Uzao wako utayamiliki ma-
taifa,

Nao watakaa katika majiji
yaliyoachwa ukiwa.^f

4 Usiogepe,^g kwa maana hu-
taaibishwa;^h

Usifedheheke, kwa maana
hutakatishwa tamaa.

Kwa maana utaisahau aibu
ya ujana wako,

Nawe hutaikumbuka tena
fedheha ya ujane wako.ⁱ

5 "Kwa maana Muumba*ⁱ
wako Mkuu ni kama
mume[#] wako,^j

Yehova wa majeshi ndilo
jina lake,

Na Mtakatifu wa Israeli ni
Mkombozi wako.^k

Ataitwa Mungu wa dunia
yote.^l

6 Kwa maana Yehova alikui-
ta kana kwamba wewe ni
mke aliyeachwa na aliye
na huzuni,^{*m}

54:1 *Au "watoto." 54:1, 5 #Au "bwa-
na mkubwa." 54:5 *Au "Mtengenezaji."
54:6 *Tnn., "aliyeumizwa rohani."

- Kama mke aliyeolewa wakati wa ujana kisha akakataliwa," asema Mungu wako.
- 7** "Kwa maana nilikuacha kwa muda mfupi, Lakini nitakukusanya tena kwa rehema nyingi.^a
- 8** Kwa furiko la hasira niliuficha uso wangu kutoka kwako kwa muda mfupi,^b Lakini nitakuonyesha rehema kwa upendo mshikamanifu wa milele,"^c asema Mkombozi^d wako, Yehova.
- 9** "Jambo hili kwangu ni kama siku za Noa.^e Kama nilivyoapa kwamba maji ya Noa hayataifunika tena dunia,^f Ndivyo ninavyoapa kwamba sitawaka hasira tena kukuelekea wewe wala kukumelea."^g
- 10** Kwa maana huenda milima ikaondolewa Na huenda vilima vikatikiswa, Lakini upendo wangu mshikamanifu hautaondolewa kwako,^h Wala agano langu la amani halitatikiswa,"ⁱ asema Yehova, Yule anayekuonyesha rehema.^j
- 11** "Ee mwanamke uliyeteseka,^k uliyerushwa na dhoruba, ambaye hajafarijiwa,^l Ninayaweka mawe yako kwa saruji ngumu Na msingi wako kwa yakuti."^m
- 12** Nitatengeneza minara yako kwa zabarijadi,

SURA YA 54

a Kum 30:1, 3
Zb 30:5
Zb 106:47
Isa 27:12
Yer 29:10

b Isa 47:6
Eze 39:23

c Isa 55:3

d Isa 48:17
Isa 49:26

e Mwa 7:23

f Mwa 8:21

g Yer 31:35, 36
Eze 39:29

h Isa 51:6

i Isa 55:3

j Isa 14:1

k Isa 52:2

l Omb 1:2, 17

m Ufu 21:19

Safu ya 2

a Yer 31:34
Yoh 6:45

b Zb 119:165
Isa 66:12
Yer 33:6

c Isa 1:26
Isa 60:21

d Isa 52:1

e Yer 23:4
Sef 3:13

f Eze 38:16, 22
Zek 2:8
Zek 12:3

g Isa 10:5

h Zb 2:2, 4
Isa 41:12

i Yer 23:6

Na malango yako kwa mawe yanayong'aa,*
Na mipaka yako yote kwa mawe yenye thamani.

- 13** Na wana* wako wote watafundishwa na Yehova,^a Na amani ya wana* wako itakuwa nyingi.^b

- 14** Utaimarishwa kabisa katika uadilifu.^c Utakuwa mbali sana na ukandamizaji,^d Hutaogopa chochote na hutakuwa na sababu yoyote ya kuhofu, Kwa maana haitakukaribia.^e

- 15** Mtu yeyote akikushambulia, Haitakuwa kwa maagizo yangu.

Yeyote anayekushambulia ataanguka kwa sababu yako."^f

- 16** "Tazama! Mimi mwenyewe nilimuumba fundi, Anayefukuta moto wa maa, Naye hutengeneza silaha kwa kazi yake. Mimi mwenyewe pia nilimuumba yule mtu mharibifu ili alete uhari-bifu."^g

- 17** Hakuna silaha yoyote itakayotokezwa dhidi yako itakayofanikiwa,^h Nawe utauhukumu ulimi wowote utakaoinuka dhidi yako katika hukumu. Huu ndio urithi wa watumishi wa Yehova, Na uadilifu wao unatoka kwangu," asema Yehova.ⁱ

54:12 * Au "mawe ya moto." 54:13 * Au "watoto."

55 Njoooni, ninyi nyote mlio na kiu,^a njoooni kwe-nye maji!^b

Ninyi msio na pesa, njoo-
ni, nunueni na mle!
Naam, njoooni, mnunue di-
vai na maziwa^c bila pesa
na bila gharama.^d

2 Kwa nini mnaendelea kuli-
pa pesa kwa ajili ya kitu
ambacho si mkate,
Na kwa nini mtumie mapa-
to yenu* kwa ajili ya kitu
ambacho hakishibishi?
Nisikilizeni kwa makini,
mle kilicho chema,^e
Nanyi mtafurahia sana
vitu vyenye lishe kweli-
kweli.^{#f}

3 Tegeni sikio na mje
kwangu.^g
Sikilizeni, nanyi mtaende-
lea* kuwa hai,
Nami nitafanya agano la
milele pamoja nanyi bila
kusita^h
Kulingana na matendo
ya upendo mshikamani-
fu kwa Daudi, ambayo ni
ya uaminifu.^{#i}

4 Tazameni! Nilimfanya awe
shahidi^j kwa mataifa,
Kiongozi^k na kamanda^l
kwa mataifa.

5 Tazama! Utaliita taifa
ambalo hulijui,
Na watu wa taifa ambao
hawajakujua watakuki-
mbilia
Kwa ajili ya Yehova Mungu
wako,^m Mtakatifu wa
Israeli,
Kwa sababu atakutukuza.ⁿ

55:2 *Au "pesa mlizopata kwa shida."
#Tnn., "mtafurahia sana unono." 55:3
*Au "nafsi yenu itaendelea." #Au "ye-
nye kuaminika; kutegemeka."

SURA YA 55

a Zb 42:2
Zb 63:1
Amo 8:11
Mt 5:6

b Isa 41:17

c Yoe 3:18

d Ufu 21:6
Ufu 22:17

e Isa 25:6

f Zb 36:7, 8
Zb 63:5

g Yak 4:8

h Isa 61:8

i 2Sa 7:8, 16
2Sa 23:5
Zb 89:28, 29
Yer 33:25, 26
Mdo 13:34

j Ufu 1:5
Ufu 3:14

k Da 9:25
Mt 23:10

l Mwa 49:10

m Zek 8:23

n Isa 49:3
Isa 60:9

Safu ya 2

a 1Nya 28:9

b Zb 145:18
Yak 4:8

c Eze 18:21
Mdo 3:19

d Kut 34:6
2Nya 33:12, 13

e Hes 14:18
Zb 103:12, 13
Isa 43:25

f Zb 40:5

g Zb 103:11

h Hes 23:19
Isa 46:11

i Yos 23:14
Isa 45:23

j Zb 135:6
Isa 46:10

k Isa 35:10

6 Mtafuteni Yehova wakati
bado anapatikana.^a
Mwiteni maadamu yuko
karibu.^b

7 Mtu mwovu na aiache njia
yake^c
Na mtu mbaya mawazo
yake;
Na arudi kwa Yehova,
ambaye atamwonyesha
reheema,^d

Kwa Mungu wetu, kwa
maana atasamehe kwa
njia kubwa.^{*e}

8 "Kwa maana mawazo ya-
ngu si mawazo yenu,^f
Na njia zenu si njia zangu,"
asema Yehova.

9 "Kwa maana kama mbingu
zilivyo juu kuliko dunia,
Ndivyo njia zangu zilivyo
juu kuliko njia zenu
Na mawazo yangu kuliko
mawazo yenu.^g

10 Kwa maana kama mvua
na theluji inavyomwagi-
ka kutoka mbinguni
Nayo hairudi huko mpaka
iiloweshe dunia na kuifa-
nya iza za na kuchipuka,
Na kumpa mbegu mpa-
ndaji na mkate yule
anayekula,

11 Hivyo ndivyo neno langu
linalotoka katika kinywa
changulitakavyokuwa.^{*h}
Halitarudi kwangu bila
matokeo,ⁱ
Bali hakika litatimiza
jambo lolote linalonipe-
ndeza,^{#j}
Na hakika litafanikiwa
katika yale ambayo ni-
melituma.

12 Kwa maana ninyi mtatoka
nje kwa shangwe,^k

55:7 *Au "kwa hiari." 55:11 *Au "lita-
thibitika kuwa." #Au "mapenzi yangu."

Nanyi mtarudishwa kwa amani.^a
 Milima na vilima vitachangamka mbele yenu kwa vigelegele vya shangwe,^b
 Na miti yote ya msituni itapiga makofi.^c

13 Badala ya vichaka vya miba, mberoshi utakua,^d
 Na badala ya upupu unao-washa, mhadasi utakua.
 Na jambo hilo litamletea Yehova sifa,^{*e}
 Ishara ya milele ambayo haitatoweka kamwe.”

56 Yehova anasema hivi:
 “Tekelezeni haki,^f na mtende uadilifu,
 Kwa maana wokovu wangu utakuja hivi karibuni
 Na uadilifu wangu utafunuliwa.^g

2 Mwenye furaha ni mtu anayefanya jambo hili
 Na mwana wa mtu anayee-ndelea kulishika kabisa,
 Anayeishika Sabato na asiyeitia unajisi^h
 Na ambaye anauzuia mkono wake usitende uovu wowote.

3 Mgeni anayejiunga na Yehovaⁱ asiseme,
 ‘Bila shaka Yehova atanitenga na watu wake.’
 Naye towashi asiseme,
 ‘Tazama! Mimi ni mti uliokauka.’”

4 Kwa maana mimi Yehova ninawaambia hivi matowashi wanaozishika sabato zangu na kuchagua mambo yanayonipendeza na kulishika kabisa agano langu:

5 “Nitawapa mnara wa ukumbusho na jina katika

SURA YA 55

a Isa 54:13
 Isa 66:12

b Isa 42:11

c Isa 44:23

d Isa 41:19
 Isa 60:13

e Yer 33:9

SURA YA 56

f Mik 6:8

g Isa 46:13
 Isa 51:5

h Isa 58:13, 14

i Isa 60:10
 Zek 8:23

Safu ya 2

a Mal 1:11

b Isa 2:3
 Mik 4:2
 Zek 8:3

c 1Fa 8:29, 43
 Mt 21:13
 Mk 11:17
 Lu 19:46

d Kum 30:3
 Isa 27:12
 Ho 1:11

e Isa 49:22
 Isa 60:4

f Yer 12:9

g Isa 6:10
 Isa 29:10

h Yer 6:13, 14
 Eze 13:16

i Eze 33:6

nyumba yangu na katika kuta zangu,
 Jambo bora kuliko wana na mabinti.

Nitawapa jina linalodumu milele,
 Ambalo halitaangamia.

6 Na wageni wanaojiunga nami Yehova ili kunihudumia,
 Kulipenda jina langu mimi Yehova^a

Na kuwa watumishi wangu,
 Wote wanaoishika Sabato na wasioitia unajisi
 Na wanaolishika kabisa agano langu,

7 Nitawaleta pia kwenye mlima wangu mtakatifu^b
 Na kuwafanya washangilie ndani ya nyumba yangu ya sala.

Dhabihu zao nzima za kuteketezwa na matoleo yao yatakubaliwa kwenye madhabahu yangu.
 Kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa ajili ya mataifa yote.”^c

8 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, anayewakusanya waliotawanyika wa Israeli,^d anasema hivi:

“Nitawakusanya wengine wajiunge naye mbali na wale ambao tayari wamekusanywa.”^e

9 Ninyi nyote wanyama wa mwituni, njooni mle,
 Ninyi nyote wanyama wa mwituni mlio msituni.^f

10 Walinzi wake ni vipofu,^g
 hakuna hata mmoja ambaye ameona.^h
 Wote ni mbwa walio bubu, wasioweza kubweka.ⁱ

Wanahemahema na kulala chini; wanapenda kulala.

11 Wao ni mbwa walafi,*
Hawashibi kamwe.

Wao ni wachungaji wasio na uelewaji.^a

Wote wamefuata njia yao wenyewe;

Kila mmoja wao anatafuta faida isiyo ya haki na ku-sema:

12 “Njoooni, acheni nichukue divai,
Na acheni tunywe kileo kingi.^b

Na kesho itakuwa kama leo, itakuwa bora hata zaidi!”

57 Mwadilifu ameangamia,
Lakini hakuna yeyote anayetia jambo hilo moyoni.

Watu washikamanifu wa-naondolewa,^{*c}

Na hakuna mtu anayeta-mbua kwamba mwadilifu ameondolewa

Kwa sababu ya[#] msiba.

2 Yeye huingia katika amani.

Wanapumzika vitandani mwao,* wote wanaote-mbea kwa unyoofu.

3 “Lakini ninyi karibieni,
Enyi wana wa mwanamke mlozi,
Ninyi watoto wa mzinzi na kahaba:

4 Mnamkejeli nani?
Ni nani mnayemfungulia kinywa wazi na kumtolea ulimi?

Je, ninyi si watoto wa ukosaji,

Watoto wa udanganyifu,^d

SURA YA 56

a Mik 3:6

b Isa 5:22
Isa 28:7
Ho 4:11

SURA YA 57

c Mik 7:2

d Isa 1:4
Isa 30:9

Safu ya 2

a Isa 1:29

b Kum 12:2
Ifa 14:22, 23

c 2Fa 16:1, 3
Yer 7:31

d Yer 3:9

e Yer 7:18

f Yer 2:20
Eze 16:16
Eze 23:17

g Eze 20:28

h Eze 16:25, 33
Eze 23:18

5 Wale wanaowaka tamaa kati ya miti mikubwa,^a

Chini ya kila mti wenye majani mengi,^b

Wanaowachinja watoto kwenye mabonde,^{*c}

Chini ya mipasuko ya majabali?

6 Mawe laini ya bondeni* ndilo fungu lako.

Naam, hayo ndiyo fungu lako.^d

Hata unayamiminia mato-leo ya kinywaji na kutoa zawadi juu yake.^e

Je, niridhike[#] na mambo hayo?

7 Ulikitayarisha kitanda chako juu ya mlima mre-fu ulioinuka,^f

Nawe ukapanda huko ili kutoa dhabihu.^g

8 Uliweka ukumbusho wako nyuma ya mlango na nyuma ya mwimo wa mlango.

Uliniacha nawe ukaji-funua;

Ulipanda huko na kukipana kitanda chako.

Nawe ukafanya agano pamoja nao.

Ulipenda kulala nao kitandani mwao,^h

Nawe ulikitazama kiungo cha kiume.*

9 Ulishuka kwa Meleki* ukiwa na mafuta

Na ukiwa na manukato mengi.

Uliwatuma wajumbe wako mbali,

57:5 *Au “makorongo.” 57:6 *Au “korongoni.” *Au “Je, nijifariji.” 57:8 *Huenda maneno hayo yanarejelea ibada ya sanamu. 57:9 *Au labda, “mfalme.”

56:11 *Au “wenye nafsi yenye nguvu.”
57:1 *Yaani, katika kifo. *Au labda,
“Kutokana na.” 57:2 *Yaani, kaburini.

- Hivi kwamba ukashuka Kaburini.*
- 10** Umejitaabisha ukifuata njia zako nyingi, Lakini hukusema, 'Hakuna matumaini!' Ulipata nguvu mpya. Ndiyo sababu hukati tamaa.*
- 11** Ulimhofu na kumwogopa nani Hivi kwamba ukaanza kusema uwongo?^a Hukunikumbuka mimi.^b Hukutia jambo lolote moyoni mwako.^c Je, sijakaa kimya na kujiondoa?^{*d} Kwa hiyo hukuniogopa mimi.
- 12** Nitatangaza 'uadilifu' wako^e na kazi zako,^f Nazo hazitakunufaisha.^g
- 13** Unapolilia msaada, Sanamu ulizojikusanyia hazitakuoka.^h Upepo utazipeperusha zote mbali sana, Zitapeperushwa na pumzi tu, Lakini yule anayenikimbi- lia atairithi nchi Naye ataumiliki mlima wangu mtakatifu.ⁱ
- 14** Itasemwa, 'Tengenezeni, tengenezeni barabara! Tayarisheni njia! Ondoeni kizuizi chochote katika njia ya watu wangu.'"
- 15** Kwa maana Yule Aliye Juu na Aliyetukuka Sana, Anayeishi* milele^k na

57:9 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 57:10 *Tnn., "huchoki." 57:11 *Au "kuficha mambo." 57:15 *Au "Anayekaa."

SURA YA 57

a Isa 30:9, 10
Isa 59:3

b Isa 1:3
Yer 2:32
Yer 9:3

c Isa 42:24, 25

d Zb 50:21

e Isa 58:2

f Isa 66:3

g Yer 7:4
Mik 3:4

h Amu 10:14
Isa 42:17

i Isa 56:6, 7
Isa 66:20
Eze 20:40
Yoe 3:17

j Isa 35:8
Isa 40:3
Isa 62:10

k Mwa 21:33
Zb 90:2
Isa 40:28
ITI 1:17

Safu ya 2

a Kut 15:11
Lu 1:46, 49

b 1Fa 8:27

c Zb 34:18
Zb 147:3
Isa 61:1
Isa 66:2

d Zb 103:9
Mik 7:18

e Ayu 34:14, 15

f Yer 6:13
Yer 8:10

g Yer 3:14

h Yer 33:6
Ho 14:4

i Isa 49:10

j Isa 12:1

k Isa 61:2
Omb 1:4

l Isa 48:18
Efe 2:17

- ambaye jina lake ni taka- tifu^a anasema hivi: "Ninaishi mahali palipo juu na patakatifu,^b Lakini ninaishi pia na wale waliopondwa na wenye roho ya unyenyekevu, Ili kuihuisha roho ya watu wa hali ya chini Na kuuhuisha moyo wa wale wanaopondwa.^c
- 16** Kwa maana sitawapinga milele Wala kuwa na hasira daima;^d Kwa sababu roho ya mwanadamu itadhoofika kwa sababu yangu,^e Hata viumbe wanaopumua ambao niliwaumba.
- 17** Nilikasirika kwa sababu alitenda dhambi kwa ku- fuatilia faida isiyo ya haki,^f Basi nikampiga, nikaufi- cha uso wangu, nami nikashikwa na hasira. Lakini aliendelea kuwa mwasi^g akifuata njia ya moyo wake.
- 18** Nimeziona njia zake, Lakini nitamponya^h na ku- mwongozaⁱ Na kumrudishia* faraja yeye^j na watu wake wa- naoomboleza."^k
- 19** "Ninaumba matunda ya midomo. Yule aliye mbali sana ata- pewa amani ya kudumu na pia yule aliye karibu,"^l asema Yehova, "Nami nitamponya."
- 20** "Lakini waovu ni kama bahari iliyochofuka ambayo haiwezi kutulia,

57:18 *Au "kufidia kwa kumpa."

Na maji yake yanaendelea kurusharusha juu magugu ya baharini na matope.

21 Hakuna amani kwa wao-vu,"^a asema Mungu wangu.

58 "Ita kwa sauti yote kutoka kooni; usijizuie!

Paza sauti yako kama pembe.

Watangazie watu wangu uasi wao,^b

Na nyumba ya Yakobo dhambi zao.

2 Wananitafuta siku baada ya siku,

Nao wanafurahia kuzijua njia zangu,

Kana kwamba walikuwa taifa lililotenda uadilifu

Na ambalo halikuacha haki ya Mungu wao.^c

Wananiomba hukumu za uadilifu,

Wakifurahia kumkaribia Mungu.^d

3 'Kwa nini huoni, tunapofunga?'^e

Na kwa nini hutambui tunapojitesa?'^f

Kwa sababu siku mnayofunga mnafuatia

mapendezi yenu wenyewe.^g

Nanyi mnawakandamiza wafanyakazi wenu.^g

4 Kufunga kwenu huishia kwenye ugomvi na vita, Nanyi mnashambulia kwa ngumi ya uovu.

Hamwezi kufunga kama mnavyofanya leo na sauti yenu isikiwe mbinguni.

58:3 *Au "tunapozitesa nafsi zetu?"
^gAu "mambo mnayofurahia."

SURA YA 57

a Met 13:9
Isa 3:11

SURA YA 58

b Isa 1:2
Isa 31:6
Isa 59:13

c Isa 29:13
Eze 33:32

d Isa 1:14, 15

e Mal 3:14

f Law 16:29

g Yer 34:15, 16
Mik 3:2-4

Safu ya 2

a Yer 34:8, 9

b Met 28:27

c Zb 41:1
Zb 112:9
Met 19:17
Met 22:9

d Eze 18:7, 8
Yak 2:15, 16
1Yo 3:17

e Met 4:18

f Kut 14:19
Isa 52:12

5 Je, kufunga ambako ninachagua kunapaswa kuwa hivi,

Siku ya mtu kujitesa,*
 Kuinamisha chini kichwa chake kama utete,

Na kufanya nguo za magunia na majivu yawe kitanda chake?

Je, huko ndiko unakoita kufunga na siku inayompendeza Yehova?

6 Hapana, huku ndiko kufunga ambako ninachagua: Kuondoa pingu za uovu, Kufungua vifungo vya nira,^a

Kuwaachilia huru waliokandamizwa,^b

Na kuivunja kila nira mara mbili;

7 Ni kumgawia aliye na njaa mkate wako,^c

Kuwaleta maskini na wasio na makao nyumbani mwako,

Kumvisha aliye uchi unapokutana naye,^d

Na kutowageuzia mgongo watu wako wa ukoo.

8 Ndipo nuru yako itakapochomoza kama mapambazuko,^e

Na oponyaji wako utatokea upesi.

Uadilifu wako utakutanguulia,

Na utukufu wa Yehova utakuwa ulinzi nyuma yako.^f

9 Kisha utaita, na Yehova atakujibu;

Utalilia msaada, naye atasema, 'Mimi hapa!'

Ukiiondoa nira kati yako Ukiacha kunyoosha

kidole chako na kuacha

58:5 *Au "kuitesa nafsi yake."

- kuongea mambo yanayo-dhuru,^a
- 10** Ukimpa mwenye njaa kile ambacho wewe mwenyewe unatamani^{*b}
Na kuwashibisha wale wa-naoteseka,[#]
Ndipo nuru yako itakapong'aa hata gizani,
Na giza lako litakuwa kama adhuhuri.^c
- 11** Yehova atakuongoza daima
Na kukushibisha* hata katika nchi iliyokauka;^d
Ataitia nguvu mifupa yako,
Nawe utakuwa kama bustani iliyonyweshwa maji vizuri,^e
Kama chemchemi ambayo maji yake hayakauki kamwe.
- 12** Watajenga upya magofu ya kale kwa sababu yako,^f
Nawe utairudisha misingi ya vizazi vilivyopita.^g
Utaitwa mrekebishaji wa kuta zilizobomoka,^{*h}
Mrekebishaji wa barabara zinazopita kwenye makao.
- 13** Ikiwa kwa sababu ya Sabato unaacha kufuatilia* mapendezi yako mwenyewe[#] katika siku yangu takatifuⁱ
Nawe uiite Sabato kuwa ni furaha tele, siku takatifu ya Yehova, siku ya kutukuzwa,^j

58:10 *Au "tamaa za nafsi yako." [#] Au "kuzishibisha nafsi zinazoteseka."
58:11 *Au "kuishibisha nafsi yako."
58:12 *Tnn., "wa mashimo yaliyo katika ukuta." **58:13** *Tnn., "unauguzwa mguu wako usifuatilie." [#] Au "mambo unayofurahia."

SURA YA 58

a Isa 32:6
Isa 59:3

b Kum 15:7, 8

c Zb 37:5, 6

d Isa 49:10

e Isa 61:11
Yer 31:12

f Ne 2:5
Yer 31:38

g Isa 61:4

h Ne 6:1
Amo 9:11, 14

i Ne 13:15
Isa 56:2
Yer 17:21

j Kum 5:12-14

Safu ya 2

a Kum 32:13

b Zb 105:10, 11
Yer 3:18

SURA YA 59

c Hes 11:23
Isa 50:2

d Zb 116:1

e Yer 5:25

f Kum 31:16, 17
Kum 32:20
Isa 57:17
Eze 39:23
Mik 3:4

g Isa 1:15
Yer 2:34
Eze 7:23

h Yer 7:9, 10
Eze 13:8

i Yer 5:1
Eze 22:30
Mik 7:2

j Isa 30:12, 13

k Mik 2:1

Nawe uitukuze badala ya kufuatilia mapendezi yako mwenyewe na kusema maneno ya upuuzi,

- 14** Ndipo utakapopata furaha tele katika Yehova,
Nami nitakufanya upande sehemu za juu za dunia.^a
Nitakufanya ule kutokana na* urithi wa Yakobo babu yako,^b
Kwa maana kinywa cha Yehova kimesema hivyo."

59 Tazama! Mkono wa Yehova si mfupi usiweze kuokoa,^c

Wala sikio lake si zito lisiweze kusikia.^d

- 2** Hapana, makosa yenu wenyewe yamewatenganisha na Mungu wenu.^e
Dhambi zenu zimemfanya aufiche uso wake kutoka kwenu,
Naye anakataa kuwasikiliza.^f

- 3** Kwa maana viganja vyenu vimechafuliwa kwa damu^g
Na vidole vyenu kwa kosa. Midomo yenu inasema uwongo,^h na ulimi wenu unanong'ona ukosefu wa uadilifu.

- 4** Hakuna yeyote anayedai uadilifu utendeke,ⁱ
Na hakuna anayeenda mahakamani akiwa na ukweli.
Wanatumaini mambo ambayo si halisi^{*j} na kusema mambo yasiyo na maana.
Wanatunga mimba ya taabu na kuzaa madhara.^k

58:14 *Au "ufurahie." **59:4** *Au "ubaitili."

- 5** Wanaangua mayai ya nyoka mwenye sumu,
Nao wanafuma utando wa buibui.^a
Yeyote anayekula mayai yao atakufa,
Na yai linalovunjwa linaangua nyoka kipiri.
- 6** Utando wao wa buibui hautatumika kama vazi,
Wala hawatajifunika kwa wanachotengeneza.^b
Kazi zao zinadhuru,
Na matendo ya ukatili yamo mikononi mwao.^c
- 7** Miguu yao hukimbilia kutenda maovu,
Nao wanafanya haraka kumwaga damu isiyo na hatia.^d
Mawazo yao ni mawazo yanayodhuru;
Njia zao zina uharibifu na maumivu.^e
- 8** Hawajaijua njia ya amani,
Na hakuna haki katika vijia vyao.^f
Wanazipotosha barabara zao;
Hakuna yeyote anayetembea humo atakayejua amani.^g
- 9** Ndiyo sababu haki iko mbali sana nasi,
Na uadilifu hautufikii na kututangulia.
Tunaendelea kutumainia nuru, lakini, tazama! kuna giza;
Kutumainia mwangaza, lakini tunaendelea kute-mbea katika utusitisi.^h
- 10** Tunapapasa-papasa tu-kiutafuta ukuta kama vipofu;
Tunaendelea kupapasa-papasa kama watu wasio na macho.ⁱ

SURA YA 59

a Ayu 8:13, 14

b Isa 57:12

c Yer 6:7
Mik 6:12d Yer 22:17
Eze 9:9
Mt 23:35

e Ro 3:15-17

f Isa 5:7
Isa 59:15
Yer 5:1
Amo 6:12
Hab 1:4

g Yer 8:15

h Isa 5:30

i Kum 28:15, 29

Safu ya 2

a Isa 1:5
Eze 5:5, 6b Yer 14:7
Ho 5:5c Ezz 9:13
Ne 9:33
Da 9:5d Isa 31:6
Isa 32:6
Yer 17:13

e Yer 5:23

f Zb 82:2
Hab 1:4

g Isa 5:22, 23

h Isa 48:1

Tunajikwaa wakati wa aduhuri kama wakati wa giza la jioni;
Miongoni mwa wenye nguvu sisi ni kama tu watu waliokufa.

- 11** Sote tunaendelea kunguruma kama dubu
Na kulia kwa huzuni kama njiwa.
Tunatumaini kupata haki, lakini hakuna haki yoyote;
Kupata wokovu, lakini uko mbali sana nasi.
- 12** Kwa maana maasi yetu ni mengi mbele zako;^a
Kila moja ya dhambi zetu inashuhudia dhidi yetu.^b
Kwa maana maasi yetu yako pamoja nasi;
Tunayajua vema makosa yetu.^c
- 13** Tumemkosea na kumkana Yehova;
Tumengeuzia mgongo Mungu wetu.
Tumesema kuhusu ukandamizaji na maasi;^d
Tumetunga uwongo na kunong'ona maneno ya uwongo kutoka moyoni.^e
- 14** Haki imerudishwa nyuma,^f
Na uadilifu unasimama mbali sana;^g
Kwa maana ukweli* umejikwaa katika kiwanja cha jiji,
Na jambo la unyoofu haliwezi kuingia.
- 15** Ukweli* umetoweka,^h
Na yeyote anayeacha ubaya anaporwa.

59:14 *Au "unyoofu." 59:15 *Au "Unyoofu."

Yehova aliona jambo hilo naye akachukizwa,*

Kwa maana hakukuwa na haki.^a

16 Aliona kwamba hakuna mtu,

Naye akashangaa kwamba hakuna yeyote aliyeingilia kati,

Basi mkono wake mwenyewe ukaleta wokovu,*

Na uadilifu wake mwenyewe ukamtegemeza.

17 Kisha akavaa uadilifu kama koti la vita

Na kofia ya chuma ya wokovu* juu ya kichwa chake.^b

Alivaa nguo za kisasi kama mavazi yake^c

Na kujifunga bidii kama koti.[#]

18 Atawathawabisha kulingana na matendo yao:^d

Ghadhabu kwa wapinzani wake, kisasi kwa maadui wake.^e

Naye atavilipa visiwa kile kinachostahili.

19 Wataliogopa jina la Yehova kuanzia magharibi

Na kuanzia mashariki wataogopa utukufu wake,

Kwa maana ataingia kama mto unaoenda kasi,

Ambao unaendeshwa na roho ya Yehova.

20 “Mkombozi^f atakuja Sanyuni,^g

Kwa wale wa Yakobo wanaoacha makosa yao,”^h asema Yehova.

21 “Lakini mimi, hili ndilo agano langu pamoja nao,”ⁱ

59:15 *Tnn., “na jambo hilo lilikuwa baya machoni pake.” **59:16** *Au “ukamletea ushindi.” **59:17** *Au “ushindi.” *Au “koti lisilo na mikono.”

SURA YA 59

a Mik 3:2

b Efe 6:17
1Th 5:8

c Kum 32:35
Zb 94:1

d Ayu 34:11
Zb 62:12
Yer 17:10

e Isa 1:24
Omb 4:11
Eze 5:13

f Isa 48:17

g Isa 62:11

h Kum 30:1-3
Ro 11:26

i Ro 11:27

Safu ya 2

SURA YA 60

a Isa 51:17
Isa 52:1

b Isa 60:19, 20

c Isa 11:10

d Isa 49:23

e Ufu 21:23, 24

f Isa 49:17, 18
Isa 54:1

g Isa 49:21, 22

h Yer 33:9

asema Yehova. “Roho yangu iliyo juu yako na maneno yangu niliyoweka kinywani mwako—hayataondolewa kutoka kinywani mwako, kutoka kinywani mwa watoto wako,* au kutoka kinywani mwa wajukuu wako,”[#] asema Yehova, “kuanzia sasa mpaka milele.”

60 “Inuka, Ee mwanamke,^a angaza nuru, kwa maana nuru yako imekuja.

Utukufu wa Yehova unakuangazia.^b

2 Kwa maana tazama! giza litaifunika dunia

Na utusitusi mzito utayaifunika mataifa;

Lakini Yehova atakuangazia,

Na utukufu wake utaonekana juu yako.

3 Mataifa yataenda kwenye nuru yako^c

Na wafalme^d kwenye fahari yako inayong’aa.^{*e}

4 Inua macho yako utazame pande zote kukuzunguka!

Wote wamekusanywa; wana kuja kwako.

Wana wako wanaendelea kuja kutoka mbali sana,^f

Na mabinti wako wakiwa wametegemezwa viunoni.^g

5 Wakati huo utaona na kung’aa,^h

Na moyo wako utadundunda na kufurika,

Kwa sababu utajiri wa bahari utaelekezwa kwako;

59:21 *Tnn., “mbegu yako.” [#]Tnn., “mbegu ya mbegu yako.” **60:3** *Au “kwenye mwangaza wa mapambazuko yako.”

Mali za mataifa zitakuja kwako.^a

6 Makundi ya ngamia yataifunika nchi yako,*

Ngamia dume wachanga wa Midiani na Efa.^b

Wote kutoka Sheba—watakuja;

Watabeba dhahabu na ubani.

Watatangaza sifa za Yehova.^c

7 Makundi yote ya Kedari^d yatakusanywa kwako.

Kondoo dume wa Nebayothi^e watakutumikia.

Watakuja kwenye madhabahu yangu wakiwa na kibali,^f

Nami nitairembesha nyumba yangu yenye utukufu.^{*g}

8 Ni nani hawa wanaokuja wakiruka kama mawingu,

Kama njiwa kwenye viota vyao?*

9 Kwa maana visiwa vitanitumaini,^h

Meli za Tarshishi zinaongoza,*

Kuwaleta wana wako kutoka mbali sana,ⁱ

Pamoja na fedha yao na dhahabu yao,

Kwa sifa ya jina la Yehova Mungu wako na ya Mtakatifu wa Israeli,

Kwa maana atakutukuzi.^{#j}

10 Wageni watazijenga kuta zako,

Na wafalme wao watakuhudumia,^k

60:6 *Tnn., "yatakufunika." 60:7 *Au "nyumba yangu ya urembo." 60:8 *Au "matundu katika nyumba ya ndege?" 60:9 *Au "kama zilivyokuwa awali." #Au "atakurembesha."

SURA YA 60

a Isa 61:6
Hag 2:7, 8

b 1Nya 1:32, 33

c Mal 1:11

d Isa 42:11

e Mwa 25:13

f Kut 29:39, 42
Isa 56:6, 7

g Hag 2:9

h Isa 51:5

i Isa 60:4
Isa 66:20

j Zb 149:4
Isa 52:1
Isa 55:5

k Ezr 7:27
Ne 2:7, 8
Isa 49:23

Safu ya 2

a Kum 30:3
Zb 30:5
Isa 54:7
Isa 57:17, 18

b Ufu 21:25, 26

c Isa 60:3, 5

d Isa 41:11

e Isa 35:1, 2

f Isa 41:19
Isa 55:13

g Zb 132:7

h Isa 62:12

i 2Nya 36:20, 21
Isa 49:14
Yer 30:17
Omb 1:4

j Isa 35:10
Isa 61:7
Yer 33:10, 11

Kwa maana nilikupiga kwa hasira yangu,

Lakini kwa kibali changu* nitakuonyesha rehema.^a

11 Malango yako yatakuwa wazi daima;^b

Hayatafungwa mchana wala usiku,

Ili kukuletea mali za mataifa,

Na wafalme wao wataoongoza.^c

12 Kwa maana taifa lolote na ufalme wowote ambao hautakutumikia utaanгамia,

Nayo mataifa yataharibiwa kabisa.^d

13 Utukufu wa Lebanoni utakuja kwako,^e

Mberoshi, mtidhari, na mvinje pamoja,^f

Ili kuparembesha mahali pangu patakatifu;

Nitapatukuza mahali pa miguu yangu.^g

14 Wana wa wale waliokukandamiza watakuja na kuinama chini mbele yako;

Wote wanaokudharau watainama chini miguuni pako,

Nao watalazimika kukuita jiji la Yehova,

Sayuni la Mtakatifu wa Israeli.^h

15 Badala ya kuwa aliyeachwa na kuchukiwa, bila yeyote kupita ndani yako,ⁱ

Nitakufanya uwe chanzo cha fahari ya milele,

Chanzo cha shangwe kwa vizazi vyote.^j

60:10 *Au "kwa nia yangu njema."

- 16** Nawe kwa kweli utakunywa maziwa ya mataifa,^a
Utanyonya matiti ya wafalme,^b
Nawe hakika utajua kwamba mimi, Yehova, ni Mwokozi wako,
Na Mwenye Nguvu wa Yakobo ni Mkombozi wako.^c
- 17** Badala ya shaba nitaleta dhahabu,
Na badala ya chuma nitaleta fedha,
Badala ya mbao, shaba, Na badala ya mawe, chuma;
Nitaweka amani kuwa wanalizi wako
Na uadilifu kuwa watu wako wanaogawa kazi.^d
- 18** Ukatili hautasikiwa tena katika nchi yako
Wala maangamizi na uharibifu katika mipaka yako.^e
Nawe utaziita kuta zako Wokovu^f na malango yako Sifa.
- 19** Kwa maana jua halitakuwa tena nuru ya mchana kwako,
Wala nuru ya mwezi haitakuangazia,
Kwa maana Yehova atakuwa nuru ya milele kwako,^g
Na Mungu wako atakuwa urembo wako.^h
- 20** Jua lako halitatuwa tena, Wala mwezi wako hautafifia,
Kwa maana Yehova atakuwa nuru yako ya milele,ⁱ
Na siku zako za kuomboleza zitakuwa zimekwisha.^j

SURA YA 60

a Isa 61:6

b Isa 49:23

c Isa 49:26

d Isa 1:26
Isa 32:1e Isa 2:4
Isa 11:9
Isa 54:14
Zek 9:8

f Isa 26:1

g Zb 36:9
Isa 60:1
Ufu 21:23
Ufu 22:5

h Zek 2:4, 5

i Zb 27:1
Zb 84:11j Isa 25:8
Isa 30:19
Isa 35:10

Safu ya 2

a Isa 43:6, 7

b Isa 44:23

SURA YA 61

c Isa 42:1
Mt 3:16d Mt 11:4, 5
Mdo 10:37, 38e Lu 4:17-21
Lu 7:22
Mdo 26:17, 18

f Isa 34:8

g Isa 25:8
Mt 5:4
Lu 6:21

h Isa 60:21

- 21** Na watu wako wote watakuwa waadilifu;
Wataimiliki nchi milele.
Wao ndio chipukizi nililopanda,
Kazi ya mikono yangu,^a ili nirembeshwe.^b
- 22** Mdogo atakuwa elfu
Na mnyonge atakuwa taifa lenye nguvu.
Mimi mwenyewe, Yehova, nitaliharakisha jambo hilo kwa wakati wake.”

61 Roho ya Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova iko juu yangu,^c

Kwa sababu Yehova alinitia mafuta niwatangazie wapole habari njema.^d

Alinituma kuyafunga majeraha ya waliovunjika moyo,

Kuwatangazia mateka uhuru

Na kutangaza kwamba macho ya wafungwa yatafunguliwa kabisa.^e

- 2** Kutangaza mwaka wa nia njema ya* Yehova
Na siku ya kisasi ya Mungu wetu,^f
Kuwarejisi wote wanaomboleza,^g
- 3** Kuwaandalia mahitaji wale wanaombolezea Sayuni,
Kuwapa vazi la kichwani badala ya majivu,
Mafuta ya furaha badala ya maombolezo,
Vazi la sifa badala ya roho iliyovunjika.
Nao wataitwa miti miku-bwa ya uadilifu,
Bustani ya Yehova, ili ku-
mtukuza.^{*h}

61:2 *Au “kibali cha.” 61:3 *Au “kurembesha.”

- 4** Watajenga upya magofu ya kale;
Watasimamisha sehemu zilizoachwa ukiwa za zamani.^a
Nao watajenga upya majiji yaliyoharibiwa,^b
Sehemu zilizoachwa ukiwa kizazi baada ya kizazi.^c
- 5** “Wageni watakuja na kuingunga mifugo yenu,
Nao watu wa nchi nyingine^d watakuwa wakulima wenu na watunzaji wa mizabibu yenu.^e
- 6** Nanyi mtaitwa makuhani wa Yehova;^f
Watawaita wahudumu wa Mungu wetu.
Mtakula mali za mataifa,^g
Nanyi mtajivunia utukufu* wao.
- 7** Badala ya aibu mtakuwa na fungu mara mbili,
Na badala ya fedheha watapiga vigelegele kwa shangwe kwa sababu ya fungu lao.
Naam, watamiliki fungu mara mbili katika nchi yao.^h
Watakuwa na shangwe milele.ⁱ
- 8** Kwa maana mimi, Yehova, ninapenda haki;^j
Ninachukia unyang’anyi na ukosefu wa uadilifu.^k
Nitawapa malipo yao kwa uaminifu,
Nami nitafanya agano la milele pamoja nao.^l
- 9** Uzao wao utajulikana* miongoni mwa mataifa^m
Na wazao wao miongoni mwa watu.

61:6 *Au “utajiri.” 61:9 *Tnn., “Mbegu yao itajulikana.”

SURA YA 61

- a Isa 49:8
Isa 51:3
- b Isa 44:26
Isa 58:12
- c Eze 36:33, 34
- d Isa 60:10
- e Isa 14:1, 2
- f Kut 19:6
- g Isa 23:17, 18
Isa 60:5, 7
- h Zek 9:12
- i Isa 35:10
- j Kum 32:4
Zb 33:5
Zb 37:28
- k Met 6:16-19
- l Isa 55:3
Yer 32:40
- m Zek 8:13

Safu ya 2

- a Isa 65:23
- b Isa 65:13
- c Isa 52:1
Ufu 21:2
- d Kut 28:39, 41
- e Isa 45:8
Isa 62:1
- f Isa 58:11
Isa 60:18
Isa 62:7

SURA YA 62

- g Zb 102:13
Zek 2:12
- h Isa 1:26
- i Isa 51:5
- j Isa 54:1
Isa 60:1
- k Isa 49:23
Isa 60:11
- l Yer 33:16

Wote wanaoawaona watawatambua,
Kwamba wao ni uzao ambao* Yehova amebarikiri.”^a

- 10** Nitashangilia sana katika Yehova.
Nafsi yangu yote itashangilia katika Mungu wangu.^b
Kwa maana amenivisha mavazi ya wokovu;^c
Amenifunika kwa joho* la uadilifu,
Kama bwana harusi anayevaa kilemba kama cha kuhani,^d
Na kama bibi harusi anayejipamba kwa mapambo yake.

- 11** Kwa maana kama dunia inavyochipusha mimea
Na kama bustani inavyochipusha vitu vilivyopandwa humo,
Ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova
Atakavyofanya uadilifu^e
na sifa zichipuke^f mbele ya mataifa yote.

- 62** Sitanyamaza kwa ajili ya Sayuni,^g
Nami sitatulia kwa ajili ya Yerusalemu
Mpaka uadilifu wake ung’ae kama mwangaza mkali^h
Na wokovu wake uwake kama mwenge.ⁱ
- 2** “Mataifa yatauona uadilifu wako, ewe mwanamke,^j
Na wafalme wote utukufu wako.^k
Nawe utaitwa kwa jina jipya,^l

61:9 *Tnn., “mbegu ambayo.” 61:10 *Au “joho lisilo na mikono.”

Ambalo kinywa cha Yehova mwenyewe kitalichagua.

- 3** Utakuwa taji la urembo mkononi mwa Yehova, Kilemba cha kifalme mkononi mwa Mungu wako.
- 4** Hutaitwa tena mwanamke aliyeachwa,^a Na nchi yako haitaitwa tena ukiwa.^b Lakini utaitwa Furaha Yangu Imo Ndani Yake,^c Na nchi yako itaitwa Aliyeolewa. Kwa maana Yehova atafurahishwa nawe, Na nchi yako itakuwa kama aliyeolewa.
- 5** Kwa maana kama kijana wa kiume anavyomwoa msichana bikira, Ndivyo wana wako watakvyo kuoa. Kama bwana harusi anavyomfurahia bibi harusi Ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia.^d
- 6** Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu. Hawapaswi kukaa kimya daima, mchana kutwa na usiku kucha. Ninyi mnaomtaja Yehova, Msipumzike,
- 7** Na msiache kamwe apumzike mpaka aliimarishe kabisa Yerusalemu, Naam, mpaka alifanye kuwa sifa ya dunia.”^e
- 8** Yehova ameapa kiapo kwa mkono wake wa kuume, kwa mkono wake wenye nguvu: “Sitawapa tena maadui wako nafaka yako iwe chakula chao,

SURA YA 62

a Isa 49:14
Isa 54:6

b Isa 32:14

c Zb 149:4
Sef 3:17

d Isa 65:18, 19
Yer 32:41

e Isa 61:11
Yer 33:9
Sef 3:19, 20

Safu ya 2

a Kum 28:49-51
Yer 5:17

b Kum 14:23
Isa 65:21, 22

c Isa 40:3
Isa 48:20

d Isa 57:14

e Ezz 1:1, 3
Isa 11:12
Isa 49:22

f Zek 9:9
Mt 21:5
Yoh 12:15

g Isa 40:9, 10
Ufu 22:12

h Zb 107:2, 3

i Isa 54:7

SURA YA 63

j Zb 137:7
Isa 34:5, 6

k Amo 1:12

Wala wageni hawatakuwanywa divai yako mpya, ambayo umetaabika kuitapata.^a

- 9** Lakini wale wanaoikusanya wataila nao watamsifu Yehova; Na wale wanaoikusanya watainywa katika nyua zangu takatifu.”^b
- 10** Piteni humo, piteni katika malango. Watayarishieni watu njia.^c Tengenezeni, tengenezeni barabara kuu. Ondoeni mawe juu yake.^d Inueni ishara* kwa ajili ya watu.^e
- 11** Tazama! Yehova ametangaza mpaka kwenye miisho ya dunia: “Mwambieni binti ya Sanyuni, “Tazama! Wokovu wako unakuja.^f Tazama! Anakuja na thababu yake, Na malipo anayotoa yako mbele zake.”^g
- 12** Wataitwa watu watakatiifu, wale waliokombolewa na Yehova,^h Nawe utaitwa Aliyetafutwa, Jiji Ambalo Halikuachwa.ⁱ
- 63** Ni nani huyu anayekuja kutoka Edomu,^j Kutoka Bosra^k akiwa na mavazi yenye rangi zinazong’aa,* Huyu aliye na mavazi ya kifahari, Anayetembea kwa nguvu zake nyingi? “Ni mimi, Yule anayesema kwa uadilifu,

62:10 *Au “nguzo ya ishara.” 63:1 *Au labda, “nyekundu nyangavu.”

- Yule aliye na nguvu nyingi za kuokoa.”
- 2** Kwa nini mavazi yako ni mekundu,
Na kwa nini mavazi yako ni kama ya mtu anayekanyaga shinikizo la divai?^a
- 3** “Nimelikanyaga pipa la divai nikiwa peke yangu. Hakuna mtu yeyote kutoka katika mataifa aliyekuwa pamoja nami. Niliendelea kuwakanyaga kwa hasira yangu, Nami niliendelea kuwakanyaga kwa ghadhabu yangu.^b Mavazi yangu yalijaa madoa ya damu yao, Nami nimezichafua nguo zangu zote.
- 4** Kwa maana siku ya kisasi imo moyoni mwangu,^c Na mwaka wa watu wangu waliokombolewa umefika.
- 5** Nilitazama, lakini hapa kuna na yeyote wa kunisaidia; Nilishangaa kwamba hakuna yeyote aliyenitegemeza. Basi mkono wangu ukani-letea wokovu,^{*d} Na ghadhabu yangu mwenyewe ikanitegemeza.
- 6** Niliwakanyaga watu kwa hasira yangu, Niliwalewisha kwa ghadhabu yangu^e Niliiwaga damu yao ardhini.”
- 7** Nitayataja matendo ya Yehova ya upendo mshikamanifu, Matendo ya Yehova yanayostahili sifa,

SURA YA 63

a Yoe 3:13
Ufu 14:19, 20
Ufu 19:15

b Isa 34:2

c Isa 34:8
Isa 35:4
Isa 61:1, 2

d Isa 51:9
Isa 52:10
Isa 59:16

e Yer 25:15, 16

Safu ya 2

a Zb 78:12
Zb 105:5

b Kut 24:7

c Kut 14:30

d Kut 3:7

e Kut 14:19
Kut 23:20

f Kum 7:8

g Kut 19:4
Kum 1:31

h Kum 9:7

i Mdo 7:51
Efe 4:30

j Law 26:14, 17
Kum 28:63

k Yer 21:5

l Kut 14:30
Isa 51:10

m Zb 77:20

n Hes 11:16, 17

o Kut 6:1, 6
Kut 15:16

p Kut 14:21, 22

- Kwa sababu ya mambo yote ambayo Yehova ametutendea,^a
- Mambo mengi mema ambayo ameitendea nyumba ya Israeli,
Kulingana na rehema zake na upendo wake mshikamanifu ulio mwingi.
- 8** Kwa maana alisema: “Kwa hakika hawa ni watu wangu, wana ambao hawatakosu kuwa washikamanifu.”^{*b}
- Basi akawa Mwokozi wao.^c
- 9** Katika taabu zao zote, yeye alitaabika.^d Na mjumbe wake binafsi^{*} akawaokoa.^e
- Kwa upendo na huruma yake aliwakomboa,^f Naye aliwainua na kuwamba siku zote za zamani.^g
- 10** Lakini waliasi^h na kuhuzunisha roho yake takatifu.ⁱ Naye akageuka na kuwa adui yao,^j Naye akawapiga vita.^k
- 11** Nao wakazikumbuka siku za zamani, Siku za Musa mtumishi wake: “Yuko wapi Yule aliyewapandisha kutoka katika bahari^l pamoja na wachungaji wa kundi lake?^m Yuko wapi Yule aliyetia ndani yake roho Yake takatifu,ⁿ
- 12** Yule aliyefanya mkono Wake mtukufu uende pamoja na mkono wa kulia wa Musa,^o Yule aliyeyatenganisha maji mbele yao^p

63:8 *Au “ambao hawatakuwa waongo.”
63:9 *Au “malaika wa uwepo wake.”

Ili kujifanyia jina la milele,^a

13 Yule aliyewafanya wate-mbee katika maji yenye mawimbi makubwa,*
Hivi kwamba wakatembea bila kujikwaa,
Kama farasi katika nchi ili-yo wazi?#

14 Kama mifugo wanavyo-teremka katika bonde tambarare,
Ndivyo roho ya Yehova ili-vyowapumzisha.”^b
Hivyo ndivyo ulivyowao-ngoza watu wako,
Ili ujijengee jina kuu.*^c

15 Tazama kutoka mbinguni uone
Kutoka kwenye makao yako yaliyo inuliwa ya utakatifu na utukufu.*
Iko wapi bidii yako na ngu-vu zako,
Shauku ya huruma#^d na rehema yako?^e
Zimeondolewa kwangu.

16 Kwa maana wewe ni Baba yetu;^f
Ingawa huenda Abrahamu asitujue
Na huenda Israeli asituta-mbue,
Wewe, Ee Yehova, ni Baba yetu.
Mkombozi wetu wa zamani za kale ndilo jina lako.^g

17 Kwa nini, Ee Yehova, unaruhusu* tutangeta-nge kutoka kwenye njia zako?
Kwa nini unaruhusu# mio-

63:13 *Au “maji yenye kina kire-fu.” #Au “nyikani.” **63:14** *Au “zuri.” **63:15** *Au “uzuri.” #Tnn., “Msukosuko wa sehemu zako za ndani.” **63:17** *Au “unatufanya.” #Tnn., “unafanya.”

SURA YA 63

a Kut 9:15, 16
Kut 14:17
Ro 9:17

b Yos 22:4

c 2Sa 7:23
Ne 9:10

d Yer 31:20

e Kum 4:31
Ne 9:17

f Kut 4:22

g Isa 41:14

Safu ya 2

a Isa 6:10

b Zb 74:2
Zb 80:14, 15

c 2Nya 36:19
Isa 64:11
Omb 1:10

SURA YA 64

d Kut 34:10

e Hab 3:6

f Zb 130:6-8
Isa 25:9
Mik 7:7
1Ko 2:9

yo yetu iwe migumu ili tusikuogope?^a

Rudi, kwa ajili ya watumi-shi wako,

Makabila ya urithi wako.^b

18 Watu wako watakatifu waliimiliki kwa muda mfupi.

Maadui wetu walipakanyaga-kanyaga mahali pako patakatifu.^c

19 Kwa muda mrefu sana tumekuwa kama watu ambao hukuwatawala kamwe,

Kama watu ambao hawa-kuitwa kamwe kwa jina lako.

64 Laiti ungezipasua mbi-ngu ushuke chini,
Ili milima itetemeke kwa sababu yako,

2 Kama moto unavyotekete-za vichaka,

Na moto huo unachemsha maji,

Basi jina lako litajulikana kwa maadui wako,

Na mataifa yatatemeka mbele zako!

3 Ulipofanya mambo ya-nayoogopesha ambayo hatungeweza kuyata-zamia,^d

Ulishuka, nayo milima ika-tetemeka mbele zako.^e

4 Tangu zamani hakuna mtu aliyesikia wala kutega sikio,

Wala hakuna jicho lili-lomwona Mungu, isipokuwa wewe,

Yule anayetenda kwa ajili ya wale wanaoendelea kumtarajia.*^f

64:4 *Au “kumngojea kwa subira.”

- 5 Umekutana na wale wa-naoshangilia kutenda mambo yanayofaa,^a Wale wanaokukumbuka na kufuata njia zako. Tazama! Ulikuwa na ghadhabu, huku sisi tukiendelea kutenda dhambi,^b Tulifanya hivyo kwa muda mrefu. Je, sasa tuokolewe?
- 6 Na sisi sote tumekuwa kama mtu asiye safi, Na matendo yetu yote ya uadilifu ni kama kita-mbaa cha hedhi.^c Sisi sote tutanyauka kama jani, Na makosa yetu yatatupe-perusha kama upepo.
- 7 Hakuna yeyote anayeliitia jina lako, Hakuna yeyote anayeji-chocha kukushika, Kwa maana umeuficha uso wako kutoka kwetu,^d Nawe unatufanya tudhoo-fike* kwa sababu ya[#] kosa letu.
- 8 Lakini sasa, Ee Yehova, wewe ni Baba yetu.^e Sisi ni udongo, nawe ni Mfinyanzi wetu;^{*f} Sisi sote ni kazi ya mkono wako.
- 9 Usiwe na ghadhabu nyi-ngi, Ee Yehova,^g Nawe usilikumbuke kosa letu milele. Tafadhali, tutazame, kwa maana sisi sote ni watu wako.
- 10 Majiji yako matakatifu yamekuwa nyika.

64:7 *Tnn., "tuyeyuke." #Tnn., "kwa mkono wa." 64:8 *Au "Muumba wetu."

SURA YA 64

a Sef 2:3
Mdo 10:34, 35

b Isa 1:21
Isa 63:10

c Law 12:2
Law 15:20

d Kum 31:17
Isa 57:17

e Isa 63:16

f Isa 29:16
Isa 45:9
Yer 18:6

g Zb 74:1
Zb 79:5

Safu ya 2

a Zb 79:1
Omb 1:4
Omb 5:18
Mik 3:12

b 2Nya 36:17, 19
Yer 52:12, 13

c Zb 74:10, 11
Zek 1:12

SURA YA 65

d Isa 55:6, 7

e Ro 10:20, 21

f Kum 31:27
Ne 9:29
Zek 7:11

g Isa 59:7, 8
Yer 35:15

h Yer 5:23

i 2Fa 17:16, 17
Yer 32:29

j Isa 1:29
Isa 66:17

k Hes 19:16

l Law 11:7, 8
Isa 66:17

Sayuni imekuwa nyika, Yerusalemu limekuwa ukiwa.^a

- 11 Nyumba yetu ya* utakati-fu na utukufu,[#] Ambamo mababu zetu wa-likusifu, Imeteketewa kwa moto,^b Na vitu vyote tulivyovitha-mini sana vimeharibiwa.
- 12 Baada ya hayo yote, je, bado utajizua, Ee Yehova? Je, utaendelea kunyamaza na kucha tuteseke kupi-ta kiasi?^c

65 "Nimeruhusu wale ambao hawakuuliza kunihusu wanitafute;

Nimeruhusu wale ambao hawakunitafuta wani-pate.^d

Nililiambia taifa ambalo halikuwa linaliitia jina langu, 'Nipo hapa, nipo hapa!'^e

- 2 Mchana kutwa nimewa-nyooshea mikonu yangu watu wakaidi,^f Wale wanaotembea katika njia isiyo nzuri,^g Wanaofuata mawazo yao wenyewe;^h
- 3 Watu wanaonikasirisha daima mbele za uso wangu,ⁱ Wanaotoa dhabihu katika bustani/ na kufukiza mo-shi wa dhabihu kwenye matofali.
- 4 Wanaketi kati ya maka-buri,^k Nao wanakaa usiku kucha mafichoni,^{*} Wakila nyama ya nguruwe,^l

64:11 *Au "Hekalu letu la." #Au "uzu-ri." 65:4 *Au labda, "katika vibanda vya kukesha."

Na mchuzi wa vitu vichafu* umo katika vyombo vyao.^a

- 5 Wanasema, 'Kaa peke yako; usinikaribie, Kwa maana mimi ni mtakatifu kuliko wewe.*'

Hawa ni moshi katika mianzi ya pua yangu, moto unaowaka mchana ku-twa.

- 6 Tazama! Imeandikwa mbele zangu; Sitasimama tuli, Lakini nitawalipa,^b Nitawalipa kikamili*'

- 7 Kwa ajili ya makosa yao na kwa ajili ya makosa ya mababu zao pia,"^c asema Yehova.

"Kwa sababu wamefukiza moshi wa dhabihu juu ya milima

Nao wamenishutumu juu ya vilima,^d

Kwanza nitawapimia mali-po yao kamili."*

- 8 Yehova anasema hivi:

"Kama divai mpya inapatikana katika kishada cha zabibu

Kisha mtu anasema, 'Usi-kiharibu, kwa sababu kuna kitu kizuri* ndani yake,'

Ndivyo nitakavyofanya kwa ajili ya watumishi wangu;

Sitawaangamiza wote.^e

- 9 Nitatoa uzao* katika Yakobo

Na katika Yuda mrithi wa milima yangu;^f

65:4 *Au "visivyo safi." 65:5 *Au labda, "Kwa maana nitakupa utakatifu wangu." 65:6, 7 *Tnn., "katika vifua vyao." 65:8 *Tnn., "kina baraka." 65:9 *Tnn., "mbegu."

SURA YA 65

a Kum 14:3

b Zb 50:3, 21
Yer 16:18
Eze 11:21

c Kut 20:4, 5
Law 26:39

d 1Fa 22:41, 43
2Fa 12:3

e Yer 30:11
Amo 9:8

f Isa 60:21
Eze 37:21
Oba 17

Safu ya 2

a Isa 61:7
Sef 3:20

b Isa 33:9

c Yos 7:24
Ho 2:15

d Isa 1:4

e 2Nya 28:24
2Nya 34:25

f Law 26:25
Eze 6:13

g Eze 9:6

h 2Nya 36:15, 16

i Isa 66:3

j Zb 37:19, 25
Amo 8:11

k Isa 49:10

Watu wangu niliowachagua wataumiliki, Na watumishi wangu wata-kaa huko.^a

- 10 Sharoni^b itakuwa malisho ya kondoo

Na Bonde la* Akori^c mahali pa kupumzika pa ng'ombe,

Kwa ajili ya watu wangu wanaonitafuta.

- 11 Lakini ninyi ni kati ya wale wanaomwacha Yehova,^d

Wanaousahau mlima wangu mtakatifu,^e

Wanaoandaa meza kwa ajili ya mungu wa Bahati Njema,

Na wale wanaovijaza vikombe divai iliyochangeanywa kwa ajili ya mungu wa Majaliwa.

- 12 Basi nitawaamulia muuawe kwa upanga,^f

Nanyi nyote mtainama chini ili mchinjwe,^g

Kwa sababu niliita, lakini hamkuitika,

Nilizungumza lakini hamkusikiliza;^h

Mliendelea kutenda maovu machoni pangu,

Nanyi mkachagua mambo yaliyonichukiza."ⁱ

- 13 Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

"Tazama! Watumishi wangu watakula, lakini ninyi mtakuwa na njaa.^j

Tazama! Watumishi wangu watakunywa,^k lakini ninyi mtakuwa na kiu.

65:10 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

Tazama! Watumishi wangu watahangilia,^a lakini ninyi mtaona aibu.^b

- 14** Tazama! Watumishi wangu watapiga vigelegele kwa shangwe kwa sababu ya hali nzuri ya moyo, Lakini ninyi mtalia kwa sababu ya maumivu ya moyo
Nanyi mtaomboleza kwa sababu ya roho iliyovunjika.

- 15** Mtaacha jina ambalo watu wangu niliowachagua watalitumia kama laana, Na Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atamuua kila mmoja wenu, Lakini atawaita watumishi wake mwenyewe kwa jina lingine;^c

- 16** Ili kila mtu anayejitafutia baraka duniani Abarikiwe na Mungu wa kweli,*
Na yeyote anayeapa kiapo duniani Aape kwa Mungu wa kweli,*^d
Kwa maana taabu za zamani zitasahauliwa;[#] Zitafichwa kutoka machoni pangu.^e

- 17** Kwa maana, tazama! ninaumba mbingu mpya na dunia mpya;^f
Na mambo ya zamani hayataingia tena akilini,*
Wala hayataingia tena moyoni.^g

- 18** Basi furahini na kushangilia milele kwa sababu ya vitu ninavyoumba.

65:16 *Au "uaminifu." Tnn., "Amina."
#Au "matatizo ya zamani yatasahauliwa."
65:17 *Au "hayatakumbukwa."

SURA YA 65

a Isa 66:14

b Isa 66:5

c Isa 62:2
Yer 33:16

d Kum 6:13

e Isa 12:1
Yer 31:12
Sef 3:14, 15f Ezr 5:2
Isa 51:16
Isa 66:22
2Pe 3:13

g Ufu 21:1, 4

Safu ya 2

a Isa 51:11

b Isa 62:4
Yer 32:41c Isa 25:8
Yer 31:12

d Yer 31:4

e Isa 62:8
Amo 9:14

f Zb 92:12-14

g Law 26:3-5
Kum 28:4

Kwa maana tazama! ninauomba Yerusalemu kuwa sababu ya shangwe
Na watu wake kuwa sababu ya furaha.^a

- 19** Nami nitashangilia kwa sababu ya Yerusalemu na kufurahi kwa sababu ya watu wangu;^b
Sauti ya kulia na ya maombolezo kwa sababu ya taabu haitasikika tena ndani yake.^c

- 20** "Hakutakuwemo tena ndani yake mtoto mchanga anayeishi siku chache tu, Wala mzee asiyetimiza siku zake.

Kwa maana mtu anayekufa akiwa na miaka mia moja ataonwa kuwa mvulana tu,

Na mtenda dhambi atalaaniwa, hata ingawa ana umri wa miaka mia moja.*

- 21** Watajenga nyumba na kuiishi ndani yake,^d
Nao watapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake.^e

- 22** Hawatajenga na mtu mwingine akae ndani yake, Wala hawatapanda na watu wengine wale.
Kwa maana siku za watu wangu zitakuwa kama siku za mti,^f

Na watu wangu niliowachagua watafurahia kikamili kazi ya mikono yao.

- 23** Hawatafanya kazi* ya bure,^g

65:20 *Au labda, "Na mtu yeyote asiyetimiza miaka mia moja ataonwa kuwa amelaaniwa."
65:23 *Au "kazi ngumu."

Wala hawatazaa watoto ili wataabike,

Kwa sababu wao ni uzao wa* watu waliobarikiwa na Yehova,^a

Na wazao wao pamoja nao.^b

24 Hata kabla hawajaita, nitajibu;

Wakiwa bado wanasema, nitasikia.

25 Mbwanawitu na mwanakondoo watalisha pamoja, Simba atakula majani kama ng'ombe dume,^c Na chakula cha nyoka kita-kuwa mavumbi.

Hawatadhuru wala kusababisha uharibifu wowote katika mlima wangu wote mtakatifu,^d asema Yehova.

66 Yehova anasema hivi: “Mbingu ni kiti changu cha ufalme, na dunia ni kiti cha miguu yangu.^e

Hivyo basi, iko wapi nyumba mnyoweza kunijengea,^f

Na pako wapi mahali pangu pa kupumzikia?”^g

2 “Sasa mkono wangu mwe-nyewe uliumba vitu hivi vyote,

Na vitu vyote vilikuja kuwapo kwa njia hiyo,” asema Yehova.^h

“Basi, nitamtazama huyu, Yule aliyemnyenyekevu na aliyevunjika rohani na anayelitetemeeke* neno langu.ⁱ

3 Anayemchinja ng'ombe dume ni kama yule anayemua mwanadamu.^j

SURA YA 65

a Isa 61:9

b Isa 66:22

c Isa 35:9
Ho 2:18

d Isa 2:3, 4
Isa 11:6-9
Mik 4:2

SURA YA 66

e Mt 5:34, 35

f 2Nya 6:18
Mdo 17:24

g 1Nya 28:2
Mdo 7:48-50

h Isa 40:26

i 2Fa 22:18, 19
Lu 18:14

j Isa 1:11

Safu ya 2

a Law 11:27

b Kum 14:8

c Law 2:1, 2

d Isa 1:13

e Kum 28:15

f Yer 7:13

g 2Fa 21:9
Isa 65:3

h Isa 5:18, 19
Isa 29:13

i Isa 65:13, 14
Yer 17:13, 18

Anayemchinja kondoo ni kama yule anayevunja shingo ya mbwa.^a

Anayetoa zawadi—kama damu ya nguruwe!^b

Anayetoa toleo la ubani la ukumbusho^c ni kama yule anayebariki kwa maneno ya uchawi.*^d

Wamechagua njia zao wenyewe,

Nao wanapenda^e mambo yanayochukiza.

4 Basi nitachagua njia za kuwaaadhibu,^e

Nami nitawaletea mambo yaleyale wanayoogopa sana.

Kwa sababu nilipoita, hakuna aliyejibu;

Nilipozungumza, hakuna aliyesikiliza.^f

Waliendelea kutenda maovu machoni pangu, Nao wakachagua kufanya mambo yaliyonichukiza.”^g

5 Sikieni neno la Yehova, ninyi mnaolitetemeeke* neno laze:

“Ndugu zenu wanaowachukia na kuwatenga kwa sababu ya jina langu, walisema, ‘Yehova na atukuzwe!’^h

Lakini atatokea na kuwaletea shangwe,

Nao ndio watakoaiibishwa.”ⁱ

6 Kuna sauti ya ghasia kutoka jijini, sauti kutoka hekaluni!

Ni sauti ya Yehova akiwalipa maadui wake kile wanachostahili.

66:3 *Au labda, “yule anayeisifu sanamu.” #Au “Na nafsi zao zinapenda.”

66:5 *Au “mnaolihangaikia.”

65:23 *Tnn., “mbegu ya.” **66:2** *Au “anayelihangaikia.”

- 7** Kabla hajawa na uchungu wa kuzaa, alizaa.^a
Kabla ya kushikwa na uchungu wa kuzaa, aliji-fungua mtoto wa kiume.
- 8** Ni nani amewahi kusikia jambo kama hilo?
Ni nani ameona mambo kama hayo?
Je, nchi itazaliwa katika siku moja?
Au, je, taifa lote litazaliwa mara moja?
Hata hivyo, mara tu Sa-yuni aliposhikwa na uchungu wa kuzaa, ali-wazaa wanawe.
- 9** “Je, nimfanye mtoto akaribie kuzaliwa kisha nifanye asizaliwe?” asema Yehova.
“Au, je, nisababishe afikie hatua ya kuzaliwa kisha nifunge tumbo la uzazi?” asema Mungu wako.
- 10** Shangilieni pamoja na Yerusalemu na mfurahi pamoja naye,^b ninyi nyote mnaompenda.^c
Furahini sana pamoja naye, ninyi nyote mnao-mwombolezea,
- 11** Kwa maana mtanyonya na kushiba kabisa maziwa ya titi lake la faraja, Nanyi mtakunywa sana na kufurahia utukufu wake mwingi.
- 12** Kwa maana Yehova anase-ma hivi:
“Tazama, ninampa amani kama mto^d
Na utukufu wa mataifa kama mto unaofurika.^e
Mtanyonya na kubebwa kiunoni,
Nanyi mtachezeshwa kwe-nye magoti yake.
- SURA YA 66**
a Isa 54:1
b Isa 44:23
c Zb 137:6
d Isa 9:7
e Isa 60:3
Hag 2:7
- Safu ya 2**
a Isa 51:3
b Isa 44:28
Isa 65:18, 19
c Isa 59:18
d Kum 4:24
e Zb 50:3
Yer 25:32, 33
f 2Th 1:7, 8
g Isa 1:29
Isa 65:3
h Law 11:7, 8
Isa 65:4
i Law 11:29

- 13** Kama mama anavyomfari-ji mwanawe,
Ndivyo nitakavyoendelea kuwafariji;^a
Nanyi mtafarijiwa kwa sa-babu ya Yerusalemu.^b
- 14** Mtaona jambo hilo, na moyo wenu utashangilia, Mifupa yenu itanawiri kama majani mabichi. Na mkono wa Yehova utajulikana* kwa watumishi wake,
Lakini atawashutumu maadui wake.”^c
- 15** “Kwa maana Yehova ata-kuja kama moto,^d
Na magari yake ya vita kama upepo wa dho-ruba,^e
Ili kulipa kwa hasira kali, Ili kukemea kwa miali ya moto.^f
- 16** Kwa maana Yehova ata-tekeleza hukumu kwa moto,
Naam, kwa upanga wake, dhidi ya wote wenye mwili;*
Na watakaouawa na Yehova watakuwa wengi.
- 17** “Wale wanaojitakasa na kujisafisha ili waingie kwenye bustani*^g wakimfuata yule aliyekatikati, wale wanaokula nyama ya nguruwe^h na vitu vinyavyochukiza na panya,ⁱ wote watafikia mwisho wao pamo-ja,” asema Yehova. **18** “Kwa kuwa ninajua kazi zao na ma-wazo yao, ninakuja kuwakusanya watu wa mataifa yote na lugha zote, nao watakuja na kuuona utukufu wangu.”
- 66:14** *Au “nguvu za Yehova zitajulikana.” **66:16** *Au “wanadamu wote.” **66:17** *Yaani, bustani za pekee zilizotumiwa kwa ajili ya ibada ya sanamu.

19 “Nitaweka ishara miongoni mwao, nami nitawapeleka baadhi ya wale wanaoponyoka waende kwa mataifa –waende Tarshishi,^a Pulu, na Ludi,^b wale wanaouvuta upinde, waende Tubali na Yavani,^c na kwenye visiwa vilivyo mbali sana—mataifa ambayo hayajasikia habari kunihusu wala kuuona utukufu wangu; nao watatanga utukufu wangu miongoni mwa mataifa.^d 20 Watawaleta ndugu zenu wote kutoka katika mataifa yote^e wawe zawadi kwa Yehova, wakiwa juu ya farasi, ndani ya magari ya vita, ndani ya magari ya kukokotwa yaliyofunikwa, juu ya nyumbu, juu ya ngamia wenye kasi, mpaka kwenye mlima wangu mtakatifu, Yerusalemu,” asema Yehova, “kama watu wa Israeli wanaavyoleta zawadi zao ndani ya nyumba ya Yehova zikiwa katika chombo safi.”

21 “Pia nitawachukua baadhi yao wawe makuhani na Walawi,” asema Yehova.

SURA YA 66

a Mwa 10:4

b Mwa 10:6, 13

c Mwa 10:2
Eze 27:12, 13d Isa 60:3
Mal 1:11e Kum 30:1-3
Isa 11:16
Isa 43:6
Isa 60:4, 9

Safu ya 2

a Isa 65:17, 18
2Pe 3:13
Ufu 21:1b Isa 65:23
Yer 31:35, 36c Zb 86:9
Zek 14:16
Mal 1:11d Isa 34:10
Mt 25:41
Mk 9:47, 48
2Th 1:9

22 “Kwa maana kama vile mbingu mpya na dunia mpya^a ninazoumba zitakavyoendelea kusimama mbele zangu,” asema Yehova, “ndivyo uzao wenu* na jina lenu litakavyoendelea kudumu.”^b

23 “Na kutoka mwezi mpya mpaka mwezi mpya na kutoka sabato mpaka sabato,

Wote wenye mwili* wataingia ili kuinama chini[#] mbele zangu,”^c asema Yehova.

24 “Nao watatoka nje na kuzitazama maiti za watu walioniasi;

Kwa maana funza walio juu yao hawatakufa, Na moto wao hautazimwa,^d Nao watakuwa kitu cha kuchukiza sana kwa watu wote.*

66:22 *Tnn., “mbegu yenu.” 66:23 *Au “Wanadamu wote.” #Au “kuabudu.” 66:24 *Tnn., “wote wenye mwili.”

YEREMIA

YALIYOMO

- 1 Yeremia awakwa kuwa nabii (1-10)
Maono ya mti wa mlozi (11, 12)
Maono ya chungu cha kupikia (13-16)
Yeremia atiwa nguvu kwa ajili ya utume wake (17-19)
- 2 Waisraeli wamwacha Yehova na kuanza kuabudu miungu mingine (1-37)
Israeli ni kama mzabibu wa kigeni (21)
Pindo za nguo zake zina madoa ya damu (34)
- 3 Kina cha uasi imani wa Israeli (1-5)

- Israeli na Yuda wana hatia ya uzinzi (6-11)
Mwito wa kutubu (12-25)
- 4 Kutubu kunaleta baraka (1-4)
Msiba utakuja kutoka kaskazini (5-18)
Uchungu wa Yeremia kuhusu msiba unaokuja (19-31)
 - 5 Watu wakataa nidhamu ya Yehova (1-13)
Wataharibiwa lakini hawataangamizwa kabisa (14-19)
Yehova awaadhibu watu (20-31)

- 6 Kuzingirwa kwa Yerusalemu kunakaribia (1-9)
Ghadhabu ya Yehova dhidi ya Yerusalemu (10-21)
Wanasema "Kuna amani!" wakati hakuna amani (14)
Watavamiwa kikatili kutoka kaskazini (22-26)
Yeremia atakuwa mpimaji wa madini (27-30)
- 7 Tumaini la uwongo katika hekalu la Yehova (1-11)
Hekalu litakuwa kama Shilo (12-15)
Ibada ya kidesturi yashutumiwa (16-34)
"Malkia wa Mbinguni" aabudiwa (18)
Kutoa watoto dhabihu huko Hinomu (31)
- 8 Watu wachagua njia inayopendwa na wengi (1-7)
Kuna hekima gani bila neno la Yehova? (8-17)
Yeremia aomboleza kwa sababu ya kuvunjika kwa Yuda (18-22)
"Je, hakuna zeri kule Gileadi?" (22)
- 9 Yeremia ahuzunika sana (1-3a)
Yehova aiadhibu Yuda (3b-16)
Nchi ya Yuda yaombolezewa (17-22)
Jigambe kuhusu kumjua Yehova (23-26)
- 10 Mungu aliye hai atofautishwa na miungu ya mataifa (1-16)
Uharibifu na uhamisho unaokuja (17, 18)
Yeremia aomboleza (19-22)
Sala ya nabii (23-25)
Mwanadamu hawezi kuongoza hatua yake mwenyewe (23)
- 11 Yuda avunja agano lake pamoja na Mungu (1-17)
Miungu mingi kama majiji (13)
Yeremia afananishwa na mwanakondoo anayepeleka machinjioni (18-20)
Yeremia apingwa na watu wa mji wa nyumbani kwao (21-23)
- 12 Yeremia alalamika (1-4)
Jibu la Yehova (5-17)
- 13 Mshipi wa kitani ulioharibika (1-11)
Mitungi ya divai itavunjwavyunja (12-14)
Watu wa Yuda wasioweza kubadilika watapeleka uhamishoni (15-27)
"Je, Mkushi anaweza kuibadili ngozi yake?" (23)
- 14 Ukame, njaa kali, na upanga (1-12)
Manabii wa uwongo washutumiwa (13-18)
Yeremia akiri dhambi za watu (19-22)
- 15 Yehova hatabadili hukumu yake (1-9)
Yeremia alalamika (10)
Jibu la Yehova (11-14)
Sala ya Yeremia (15-18)
Apata furaha kwa kula maneno ya Mungu (16)
Yehova amtia nguvu Yeremia (19-21)
- 16 Yeremia hapaswi kuoa, kuomboleza, wala kusherehekea (1-9)
Adhabu, kisha kurudishwa (10-21)
- 17 Dhambi ya Yuda imetia mizizi (1-4)
Baraka za kumtumaini Yehova (5-8)
Moyo wenye hila (9-11)
Yehova, tumaini la Israeli (12, 13)
Sala ya Yeremia (14-18)
Kuishika Sabato ikiwa siku takatifu (19-27)
- 18 Udongo mikononi mwa mfanyanzi (1-12)
Yehova awageuzia Israeli mgongo (13-17)
Njama dhidi ya Yeremia; ombi lake (18-23)
- 19 Yeremia aambiwa avunje chupa ya udongo (1-15)
Kumtolea Baali dhabihu za watoto (5)
- 20 Pashuri ampiga Yeremia (1-6)
Yeremia hawezi kuacha kuhubiri (7-13)
Ujumbe wa Mungu ni kama moto unaowaka (9)
Yehova ni kama shujaa anayetisha (11)
Yeremia alalamika (14-18)
- 21 Yehova akataa ombi la Sedekia (1-7)
Watu kuchagua uzima au kifo (8-14)
- 22 Ujumbe wa hukumu dhidi ya wafalme waovu (1-30)
Kumhusu Shalumu (10-12)
Kumhusu Yehoyakimu (13-23)
Kumhusu Konia (24-30)
- 23 Wachungaji wazuri na wabaya (1-4)
Usalama chini ya "chipukizi adilifu" (5-8)
Manabii wa uwongo washutumiwa (9-32)
"Mzigo" wa Yehova (33-40)
- 24 Tini nzuri na tini mbaya (1-10)

- 25 Kesi ya Yehova dhidi ya mataifa (1-38)
Mataifa yatatumikia Babiloni kwa miaka 70 (11)
Kikombe cha divai ya ghadhabu ya Mungu (15)
Msiba kutoka taifa moja hadi lingine (32)
Wale ambao Yehova atawaua (33)
- 26 Maadui watishia kumuua Yeremia (1-15)
Yeremia aokolewa (16-19)
Unabii wa Mika wanukuliwa (18)
Nabii Uriya (20-24)
- 27 Nira ya Babiloni (1-11)
Sedekia aambiwa ajitiishe kwa Babiloni (12-22)
- 28 Nabii wa uwongo Hanania ampinga nabii Yeremia (1-17)
- 29 Barua ya Yeremia kwa watu walio uhamishoni Babiloni (1-23)
Waisraeli watarudi baada ya miaka 70 (10)
Ujumbe kwa Shemaya (24-32)
- 30 Ahadi za kurudishwa na kuponywa (1-24)
- 31 Waisraeli waliobaki wataishi tena nchini (1-30)
Raheli awaombolezea watoto wake (15)
Agano jipya (31-40)
- 32 Yeremia anunua shamba (1-15)
Sala ya Yeremia (16-25)
Jibu la Yehova (26-44)
- 33 Ahadi ya kurudishwa (1-13)
Usalama chini ya “chipukizi adilifu” (14-16)
Agano pamoja na Daudi na makuhani (17-26)
Agano kuhusu mchana na usiku (20)
- 34 Ujumbe wa hukumu kwa Sedekia (1-7)
Agano la kuwachilia huru watumwa lavunjwa (8-22)
- 35 Warekabu waonyesha utii wa pekee (1-19)
- 36 Yeremia asema mambo kisha yaandikwa katika kitabu cha kukunjwa (1-7)
Baruku asoma kwa sauti kitabu cha kukunjwa (8-19)
Yehoyakimu akichoma moto kitabu hicho cha kukunjwa (20-26)
- Ujumbe waandikwa tena kwenye kitabu kipyua cha kukunjwa (27-32)
- 37 Wakaldayo wataondoka kwa muda mfupi tu (1-10)
Yeremia afungwa gerezani (11-16)
Sedekia akutana na Yeremia (17-21)
Yeremia apewa mkate (21)
- 38 Yeremia atupwa ndani ya tangi (1-6)
Ebed-meleki amwokoza Yeremia (7-13)
Yeremia amsihi Sedekia ajisalisimisha (14-28)
- 39 Kuanguka kwa Yerusalemu (1-10)
Sedekia akimbia kisha akamatwa (4-7)
Yeremia atalindwa (11-14)
Uhui wa Ebed-meleki utaokolewa (15-18)
- 40 Nebuzaradani amwachilia huru Yeremia (1-6)
Gedalia awekwa kuwa msimamizi nchini (7-12)
Njama dhidi ya Gedalia (13-16)
- 41 Ishmaeli amua Gedalia (1-10)
Yohanani amfanya Ishmaeli akimbia (11-18)
- 42 Watu wamwomba Yeremia asali ili wapate mwongozo (1-6)
Yehova ajibu hivi: “Msiende Misri” (7-22)
- 43 Watu wakataa kutii kisha waenda Misri (1-7)
Neno la Yehova kwa Yeremia nchini Misri (8-13)
- 44 Msiba watabiriwa dhidi ya Wayahudi walio Misri (1-14)
Watu wakataa onyo la Mungu (15-30)
“Malkia wa Mbinguni” aabudiwa (17-19)
- 45 Ujumbe wa Yehova kwa Baruku (1-5)
- 46 Unabii dhidi ya Misri (1-26)
Misri itashindwa na Nebukadneza (13, 26)
Ahadi kwa Israeli (27, 28)
- 47 Unabii dhidi ya Wafilisti (1-7)
- 48 Unabii dhidi ya Moabu (1-47)
- 49 Unabii dhidi ya Amoni (1-6)
Unabii dhidi ya Edomu (7-22)
Nchi ya Edomu haitakuwa taifa tena (17, 18)
Unabii dhidi ya Damasko (23-27)
Unabii dhidi ya Kedari na Hasori (28-33)
Unabii dhidi ya Elamu (34-39)

- 50 Unabii dhidi ya Babiloni (1-46)
 Kimbieni kutoka Babiloni (8)
 Watu wa Israeli watarudishwa (17-19)
 Maji ya Babiloni yatakaushwa kabisa (38)
 Babiloni halitakaliwa tena (39, 40)
- 51 Unabii dhidi ya Babiloni (1-64)
 Babiloni litashindwa ghafla na Wamedi (8-12)

- Kitabu chatupwa ndani ya Mto Efrati (59-64)
- 52 Sedekia aasi Babiloni (1-3)
 Nebukadneza azingira Yerusalemu (4-11)
 Kuharibiwa kwa jiji na hekalu (12-23)
 Watu wapeleka uhamishoni Babiloni (24-30)
 Yehoyakini aachiliwa huru kutoka gerezeni (31-34)

1 Haya ndiyo maneno ya Y-remia* mwana wa Hilikia, mmoja wa makuhani wa Anathothi^a katika nchi ya Benjamini. **2** Neno la Yehova lilimjia katika siku za Yosia^b mwana wa Amoni,^c mfalme wa Yuda, katika mwaka wa 13 wa utawala wake. **3** Pia lilikuja katika siku za Yehoyakimu^d mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, hadi mwishoni mwa mwaka wa 11 wa utawala wa Sedekia^e mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, mpaka Yerusalemu lilipoenda uhamishoni katika mwezi wa tano.^f

4 Neno la Yehova lilinijia, likisema:

5 “Kabla sijakuumba tumboni nilikujua,^g

Na kabla hujazaliwa^h nilikutakasa.^h

Nilikufanya uwe nabii kwa mataifa.”

6 Lakini nikasema: “Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova!

Mimi sijui kuzungumza,ⁱ kwa maana mimi ni mvulana* tu.”^j

1:1 *Huenda jina hili linamaanisha “Yehova Huinua.” 1:5 *Au “nilikuchagua.”
^hTnn., “kabla hujatoka tumboni.” ^hAu “nilikuweka kando.” 1:6 *Au “kijana.”

SURA YA 1

a Yos 21:8, 18

b 2Fa 22:1, 2

c 2Fa 21:19, 20

d 2Fa 24:1
 2Nya 36:4

e 2Fa 24:18, 19

f 2Fa 25:8, 11
 Yer 52:12, 15

g Amu 13:5
 Zb 139:15, 16

h Lu 1:13, 15

i Kut 4:10

j 1Fa 3:5, 7

Safu ya 2

a Kut 7:1, 2

b Eze 2:6

c Kut 3:11, 12
 Yer 15:20
 Mdo 18:9, 10

d Isa 6:7

e Kut 4:12, 15
 Eze 33:7

f Yer 18:7-10
 Yer 24:5, 6

7 Kisha Yehova akaniambia: “Usiseme, ‘Mimi ni mvulana tu.’

Kwa maana ni lazima uende kwa wote nita-kaokutuma kwao,

Nawe unapaswa kusema kila jambo nitakalokuamuru.^a

8 Usiogope kwa sababu ya jinsi wanavyoonekana,^b

Kwa maana ‘mimi niko pamoja nawe ili nikuokoe,’^c asema Yehova.”

9 Kisha Yehova akaunyoo- sha mkono wake na kugusa kinywa changu.^d Na Yehova akaniambia: “Nimeyatia maneno yangu kinywani mwako.^e

10 Tazama, nimekutuma leo hii ili uwe juu ya mataifa na juu ya falme, ili kung’oa na kubomoa, ili kuangamiza na kuangusha, ili kujenga na kupanda.”^f

11 Neno la Yehova likanijia tena, likisema: “Unaona nini, Yeremia?” Basi nikasema: “Ni-naona tawi la mti wa mlozi.”*

12 Yehova akaniambia: “Uko sahihi, kwa maana niko macho kabisa kuhusu neno langu ili kulitimiza.”

1:11 *Tnn., “yule anayeamka.”

13 Neno la Yehova likanijia mara ya pili, likisema: “Unao-na nini?” Basi nikasema: “Ni-naona chungu* kinachoche-mka,[#] na mdomo wake ume-inama kutoka kaskazini.”

14 Kisha Yehova akaniambia: “Msiba utafunguliwa kuto-ka kaskazini
Dhidi ya wakaaji wote wa nchi.^a

15 Kwa maana ‘ninaziita fa-milia zote za falme za kaskazini,’ asema Ye-hova,^b

‘Nao watakuja; kila mmoja ataweka kiti chake cha ufalme

Kwenye malango ya Yeru-salemu,^c

Dhidi ya kuta zake pande zote

Na dhidi ya majiji yote ya Yuda.^d

16 Nami nitatangaza hukumu zangu dhidi yao kwa sa-babu ya uovu wao wote, Kwa sababu wameniacha,^e Nao wanaifukizia miungu mingine moshi wa dha-bihu^f

Na kuziinamia kazi za mi-kono yao wenyewe.^g

17 Lakini unapaswa kuwa ta-yari kuchukua hatua,^{*} Nawe unapaswa kusima-ma na kuwaambia kila jambo ninalokuamuru.

Usiwaogope,^h

Ili nisikuogopeshe mbele yao.

18 Kwa maana leo nimekufa-nya uwe jiji lenye ngome,

1:13 *Au “chungu cha kupikia chenye mdomo mpana.” #Tnn., “kinachopuli-ziwa,” kuonyesha moto unaochoche-wa chini yake. 1:17 *Tnn., “kujifunga kiuno.”

SURA YA 1

a Yer 6:1
Yer 10:22

b Yer 5:15
Yer 6:22
Yer 25:9

c Yer 39:3

d Kum 28:52
Yer 34:22
Yer 44:6

e Yos 24:20
2Fa 22:17
2Nya 7:19, 20

f Eze 8:10, 11
Ho 11:2

g Isa 2:8

h Eze 2:6

Safu ya 2

a Yer 15:20
Yer 22:11
Eze 3:8
Mik 3:8

b Yer 26:12

c Mwa 28:15
Kut 3:12
Yos 1:5

SURA YA 2

d Ho 2:15

e Kut 24:3

f Kum 2:7

g Kut 19:6
Kum 7:6

h Kut 17:8, 13

i Isa 5:4
Mik 6:3

j Kum 32:21

k Zb 115:4, 8

Nguzo ya chuma, na kuta za shaba dhidi ya nchi yote,^a

Kuelekea wafalme wa Yuda na wakuu wake, Kuelekea makuhani wake na watu wa nchi.^b

19 Nao hakika watapigana nawe, Lakini hawatakushinda, Kwa maana ‘Mimi niko pamoja nawe,’^c asema Yehova, ‘ili nikuokoe.’”

2 Neno la Yehova likanijia, likisema: **2** “Nenda ukata-ngaze masikioni mwa watu wa Yerusalemu, ‘Yehova anase-ma hivi:

“Ninakumbuka vema bidii yako* ulipokuwa kijana,^d

Upendo ulioonyesha ulipochumbiwa ili ku-olewa,^e

Jinsi ulivyoniufuata nyi-kani,

Katika nchi ambayo haipa-ndwi mbegu.^f

3 Israeli alikuwa mtakatifu kwa Yehova,^g mavuno ya kwanza ya mazao yake.” ‘Yeyote aliyemrarua aliku-wa na hatia.

Msiba ulimpata,’ asema Ye-hova.”^h

4 Sikieni neno la Yehova, enyi watu wa nyumba ya Yakobo, Nanyi familia zote za nyu-mba ya Israeli.

5 Yehova anasema hivi: “Mababu zenu waliona kosa gani kwangu,ⁱ

Hivi kwamba wakatanga-tanga mbali sana nami, Wakazifuata sanamu za ubatili,^j nao wenyewe wakawa ubatili?^k

2:2 *Au “upendo wako mshikamanifu.”

- 6** Hawakuuliza, 'Yehova yuko wapi, Yule aliyettoa nchini Misri,^a Aliyetuongoza kupitia nyikani, Kupitia nchi yenye majangwa^b na mashimo, Kupitia nchi yenye ukame^c na kivuli kizito, Kupitia nchi ambayo hakuna mtu anayesafiri humo Na ambamo hakuna mwanaadamu anayeishi?'
- 7** Kisha nikawaleta ninyi katika nchi yenye mashamba ya matunda, Ili mle matunda yake na vitu vyake vyema.^d Lakini mliingia humo na kuitia unajisi nchi yangu; Mkaufanya urithi wangu kuwa kitu kinachochukiza.^e
- 8** Makuhani hawakuuliza, 'Yehova yuko wapi?'^f Wale wanaoshughulika na Sheria hawakunijua, Wachungaji waliniasi,^g Manabii walitabiri kupitia Baali,^h Nao wakawafuata wale ambao hawangewafaidi hata kidogo.
- 9** 'Basi nitapambana zaidi nanyi,ⁱ asema Yehova, 'Nami nitapambana na wana wa wana wenu.'
- 10** 'Lakini vukeni mpaka nchi za pwani za * Kitimu^j mwone. Naam, tumeni watu Kedari^k nanyi mfikirie kwa uangalifu; Mwone ikiwa jambo kama hili limewahi kutendeka.

2:10 *Au "visiwa vya."

SURA YA 2

a Kut 14:30

b Kum 1:1
Kum 32:9, 10

c Kum 8:14, 15

d Hes 13:26, 27
Kum 6:10, 11
Kum 8:7-9

e Law 18:24
Hes 35:33
Zb 78:58
Zb 106:38
Yer 16:18

f 1Sa 2:12
Omb 4:13

g Eze 34:7, 8

h 1Fa 18:19
Yer 23:13

i Eze 20:35
Mik 6:2

j Mwa 10:2, 4

k Mwa 25:13
Zb 120:5
Yer 49:28

Safu ya 2

a Zb 106:20

b Zb 36:9
Yer 17:13
Ufu 22:1

c Isa 5:29
Yer 4:7

d Yer 46:19

e Yer 43:4, 7
Yer 46:14
Eze 30:18

f 1Nya 28:9
2Nya 7:19, 20

- 11** Je, taifa limewahi kubadili miungu yake kwa ajili ya miungu ambayo si miungu?

Lakini watu wangu mwenyewe wamebadili utukufu wangu kwa ajili ya kitu kisicho na maana.^a

- 12** Tazameni jambo hili kwa mshangao, enyi mbingu; Tetemekeneni kwa hofu kubwa,' asema Yehova,

- 13** 'Kwa sababu watu wangu wamefanya mambo mawili mabaya:

Wameniacha mimi, chemchemi ya maji yaliyo hai,^b

Na kujichimbia* matangi ya maji,

Matangi yaliyovunjika, ambayo hayawezi kuhifadhi maji.'

- 14** 'Je, Israeli ni mtumishi, au ni mtumwa aliyezaliwa nyumbani?

Basi kwa nini amekuwa kitu cha kuporwa?

- 15** Wanasimba* wananguruma dhidi yake;^c

Wameinua sauti zao.

Waliifanya nchi yake kuwa kitu cha kutisha.

Majiji yake yametekezwa, hivi kwamba hakuna mkaaji.

- 16** Watu wa Nofu*^d na Tahpanesi^e wanakula utosi wa kichwa chako.

- 17** Je, hukujiletea jambo hilo Kwa kumwacha Yehova Mungu wako^f

2:13 *Au "kuchonga," inaelekea kwenye mwamba. 2:15 *Au "Wanasimba wenyewe manyoya marefu shingoni." 2:16 *Au "Memfisi."

- Alipokuwa akikuongoza njiani?
- 18** Sasa kwa nini unatamani njia ya kwenda Misri^a Ili kunywa maji ya Shihori?^{*}
Kwa nini unatamani njia ya kwenda Ashuru^b Ili kunywa maji ya ule Mto?^z
- 19** Uovu wako unapaswa kukurekebisha, Na ukosefu wako wa uaminifu unapaswa kukukaripia.
Jua na utambue ubaya na uchungu^c wa Kumwacha Yehova Mungu wako;
Hujaniogopa,^d asema Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi.
- 20** 'Kwa maana zamani niliivunja nira yako^e Na kuzikata pingu zako. Lakini ulisema: "Mimi sitatumikia,"
Kwa maana juu ya kila kilingi kirefu na chini ya kila mti wenye majani mengi^f
Ulilala ukiwa umejinyoosha, ukifanya ukahaba.^g
- 21** Nilikupanda kama mزابو wote ukiwa mbegu safi; Basi umebadilikaje na kuwa machipukizi yaliyoharibika ya mzabubu wa kigeni mbele zangu?^h
- 22** 'Hata ukioga kwa magadi na kutumia sabuni nyingi, Bado hatia yako itakuwa doa mbele zangu,ⁱ

2:18 *Yaani, kijito cha Mto Nile. ^zYaani, Mto Efrati.

SURA YA 2

a Isa 30:2
Isa 31:1
Omb 5:6
Eze 16:26
Eze 17:15

b 2Fa 16:7
Ho 5:13

c Yer 4:18

d Yer 5:22

e Law 26:13

f 1Fa 14:22, 23
Eze 6:13

g Kut 34:15
Eze 16:15, 16

h Kut 15:17
Zb 80:8
Isa 5:1

i Isa 5:4

j Yer 16:17

Safu ya 2

a Yer 18:12

b Isa 2:6
Yer 3:13

c Yer 44:17

d Ezr 9:7

- asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.
- 23** Unawezaje kusema, 'Sijajichafua.
Sijafuata Mabaali?
Angalia njia yako bondeni. Fikiria ulichofanya.
Wewe ni kama ngamia jike mchanga anayekimbia kasi,
Anayekimbia huku na huku bila mwelekeo kati ka njia zake,
- 24** Punda wa mwituni aliyezoea nyika,
Anayenusu upepo katika tamaa yake.^{*}
Ni nani anayeweza kumzuia anaposhikwa na nyege?
Hakuna yeyote kati ya wale wanaomtafuta atakayelazimika kujichosha. Watampata katika majira yake.^z
- 25** Izuie miguu yako isitembee bila viatu
Na koo lako lisiwe na kiu. Lakini ulisema, 'Hakuna tumaini lolote!^a
Hakuna! Nimewapenda wageni,^{*b}
Nami nitawafuata.^c
- 26** Kama aibu ya mwizi anapokamatwa,
Ndivyo watu wa nyumba ya Israeli walivyoaibishwa,
Wao, wafalme wao na wakuu wao,
Makuhani wao na manabii wao.^d
- 27** Wanauambia mti, 'Wewe ni baba yangu,^e
Na jiwe, 'Wewe ulinizaa.'

2:24 *Au "katika tamaa ya nafsi yake."
^zTnn., "mwezi wake." 2:25 *Au "Nimeipenda miungu ya kigeni."

e Isa 44:13

- Lakini wamenigeuzia mimi
mgongo wao badala ya
uso wao.^a
Watakapopatwa na msiba
watasema,
'Simama utuokoe!'^b
- 28** Sasa iko wapi miungu
yako uliyojitengenezea?^c
Na isimame ikiwa inaweza
kukuokoa anapopatwa
na msiba.
Kwa maana miungu yako
imekuwa mingi kama
majiji yako, Ee Yuda.^d
- 29** 'Kwa nini unaendelea ku-
shindana nami?
Kwa nini nyote mmenia-
si?'^e asema Yehova.
- 30** Nimewapiga wana wenu
bila matokeo.^f
Hawakukubali nidhamu
yoyote;^g
Upanga wenu wenyewe
uliwaangamiza manabii
wenu,^h
Kama simba anayesha-
mbulia.
- 31** Enyi kizazi hiki, fikirieni
wenyewe neno la Yehova.
Je, nimekuwa kama nyika
kwa Israeli
Au nchi yenye giza linalo-
kandamiza?
Kwa nini watu hawa, watu
wangu, wamesema, 'Tu-
nazurura kwa uhuru.
Hatutakuja kwako tena?'ⁱ
- 32** Je, bikira anaweza kuya-
sahau mapambo yake,
Na bibi harusi mavazi yake
ya kifuani?^{*}
Lakini watu wangu wame-
nisahau mimi kwa siku
zisizohesabika.^j
- 33** Ewe mwanamke, jinsi una-
vyotayarisha njia yako

2:32 *Au "ukumbuu wake wa harusi?"

SURA YA 2

a 2Nya 29:6
Yer 32:33

b Amu 10:13-15
Zb 78:34
Zb 106:47
Isa 26:16
Ho 5:15

c Kum 32:37, 38

d Yer 11:13

e Yer 5:1
Yer 9:2
Da 9:11

f 2Nya 28:20-22
Isa 9:13

g Isa 1:5
Yer 5:3
Sef 3:2

h 2Nya 36:15, 16
Ne 9:26
Mdo 7:52

i Kum 32:15

j Zb 106:21
Isa 17:10
Yer 18:15
Ho 8:14

Safu ya 2

a 2Nya 33:9

b 2Fa 21:16
Zb 106:38
Isa 10:1, 2
Mt 23:35

c Kut 22:2

d Isa 30:3
Yer 37:7

e 2Nya 28:20, 21

f 2Sa 13:19

SURA YA 3

g Isa 24:5
Yer 2:7

h Yer 2:20
Eze 16:28, 29

kwa ustadi ili kutafuta
upendo!
Umejizoeza katika njia za
uovu.^a

- 34** Hata pindo za nguo zako
zina madoa ya damu ya
maskini* wasio na
hatia,^b

Ingawa sikuwapata waki-
vunja ili kuingia;
Imejaa kwenye pindo zako
zote.^c

- 35** Lakini unasema, 'Sina
hatia.
Hakika hasira yake ime-
niondokea.'

Sasa ninaleta hukumu
dhidi yako
Kwa sababu unasema,
'Sijatenda dhambi.'

- 36** Kwa nini unaiona njia
yako isiyo thabiti kuwa
jambo dogo?

Utaona aibu kwa sababu
ya Misri pia,^d
Kama vile ulivyoona aibu
kwa sababu ya Ashuru.^e

- 37** Kwa sababu hiyo pia uta-
toka mikono yako ikiwa
juu ya kichwa chako,^f

Kwa maana Yehova
amewakataa wale
unaowategemea;
Hawatakuletea mafani-
kio."

- 3** Watu huuliza: "Mtu aki-
mfukuza mke wake naye
aondoke na kuchukuliwa na
mwanamume mwingine, je,
mtu huyu anapaswa kumrudia
tena?"

Je, nchi hiyo haijachafuli-
wa kabisa?^g

"Umefanya ukahaba na
marafiki wengi,^h

Na je, sasa unapaswa

2:34 *Au "nafsi za maskini."

kurudi kwangu?" asema Yehova.

- 2 "Inua macho yako kuelekea vilima vitupu uone. Ni wapi ambapo hukubakwa?"

Ulikaa kando ya barabara kwa ajili yao, Kama mtu anayehamama* nyikani. Unaendelea kuichafua nchi

Kwa ukahaba wako na uovu wako.^a

- 3 Kwa hiyo manyunyuyu ya mvua yamezuiwa,^b Na hakuna mvua ya masika.

Una uso wenye* ushupavu kama mwanamke anayefanya ukahaba;

Umekataa kuona aibu.^c

- 4 Lakini sasa unaniambia kwa sauti kubwa, 'Baba yangu, wewe ni rafiki yangu tangu ujana wangu!^d

- 5 Je, mtu anapaswa kuendelea kuwa na uchungu milele,

Au kuwa na kinyongo siku-zote?"

Unasema hivyo,

Lakini unaendelea kufanya mambo yote maovu unayoweza kufanya."^e

6 Katika siku za mfalme Yosia,^f Yehova aliniambia: "Je, umeona mambo ambayo Israeli asiye mwaminifu ametenda? Amepanda juu ya kila mlima mrefu na kwenda chini ya kila mti wenye majani mengi ili afanye ukahaba.^g 7 Hata baada ya kufanya mambo hayo

3:2 *Tnn., "Mwarabu." 3:3 *Tnn., "paji lenye."

SURA YA 3

a Eze 16:16
Eze 20:28

b Law 26:19
Yer 14:4
Amo 4:7

c Yer 6:15

d Yer 2:2

e Mik 2:1
Mik 7:3

f 2Fa 22:1

g Eze 20:28
Ho 4:13

Safu ya 2

a 2Fa 17:13
2Nya 30:6
Ho 14:1

b Eze 16:46
Eze 23:2, 4

c Kum 24:1

d Eze 23:4, 5, 9
Ho 2:2
Ho 9:15

e 2Fa 17:19
Eze 23:4, 11

f Isa 57:5, 6
Yer 2:27

g Eze 16:51
Eze 23:4, 11

h 2Fa 17:6
Yer 23:8

i Yer 4:1
Eze 33:11
Ho 14:1

j Ho 11:8, 9

yote, niliendelea kumwambia arudi kwangu,^a lakini hakurudi; na Yuda akaendelea kumtazama dada yake mwenye hila.^b

8 Nilipoona hivyo, nikamfukuza Israeli asiye mwaminifu akiwa na cheti kamili cha talaka^c kwa sababu ya uzinzi wake.^d Lakini Yuda dada yake mwenye hila hakuogopa; yeye pia alienda na kufanya ukahaba.^e 9 Aliona ukahaba wake kuwa jambo dogo, naye akaendelea kuichafua nchi na kufanya uzinzi na mawe na miti.^f 10 Licha ya hayo yote, Yuda dada yake mwenye hila hakurudi kwangu kwa moyo wake wote, bali kwa kujifanya tu,' asema Yehova."

11 Kisha Yehova akaniambia: "Israeli asiye mwaminifu amekuwa mwadilifu kuliko Yuda mwenye hila.^g 12 Nenda uitangazie kaskazini maneno haya:^h

"“Rudi, Ee Israeli mwasi," asema Yehova.ⁱ "Sitakutazama kwa hasira,^j kwa maana mimi ni mshikamanifu," asema Yehova." "Sitaendelea kuwa na kinyongo milele. 13 Ila tu ukubali hatia yako, kwa maana umemwasi Yehova Mungu wako. Uliendelea kutawanya wema wako* kwa wageni^k chini ya kila mti wenye majani mengi, lakini hukuitii sauti yangu," asema Yehova."

14 "Rudini, enyi wana waa-si," asema Yehova. "Kwa maana nimekuwa bwana wenu* wa kweli; nami nitawachukua, mmoja kutoka katika jiji moja na wawili kutoka kati-

3:12 *Tnn., "Sitaufanya uso wangu unguke juu yako." 3:13 *Tnn., "njia zako." #Au "miungu ya kigeni." 3:14 *Au labda, "mume wenu."

ka familia moja, nami nitawaleta Sayuni.^a **15** Nami nita-wapa wachungaji wanaoupe-ndeza moyo wangu,^b nao watawalisha kwa ujuzi na ufa-hamu. **16** Mtakuwa wengi nanyi mtazaa matunda nchi-ni siku hizo,” asema Yehova.^c “Hawatasema tena, ‘Sanduku la agano la Yehova!’ Halitaingia moyoni, wala hawatalikumbuka au kulitamani, nalo halitatengenezwa tena. **17** Wakati huo wataliita Yerusalem kiti cha ufalme cha Yehova;^d na mataifa yote yataku-sanywa pamoja kwa jina la Yehova katika Yerusalem,^e nao hawatafuata tena kwa ukaidi moyo wao mwovu.”

18 “Siku hizo watatembea pamoja, nyumba ya Yuda kando ya nyumba ya Israeli,^f na pamoja watatoka katika nchi ya kaskazini na kuingia katika nchi niliyowapa mababu zenu kuwa urithi.^g **19** Nami nilifikiri, ‘Jinsi nilivyokuweka kati ya wana na kukupa nchi inayotamanika, urithi maridadi zaidi kati ya mataifa!’^h Pia nilifikiri mtaniita ‘Baba yangu!’ na kwamba hamtageuka na kuacha kunifuata.’ **20** ‘Kwa kweli kama mke anavyomwacha mume wake* kwa hila, ninyi pia, enyi watu wa nyumba ya Israeli, mmenitendea kwa hila,ⁱ asema Yehova.”

21 Sauti imesikika kwenye vilima vilivyo vitupu, Kulia na kusihi kwa watu wa Israeli, Kwa maana wameipotoshan nja yao; Wamemsahau Yehova Mungu wao.^j

3:19 *Tnn., “majeshi ya mataifa.” 3:20 *Tnn., “mwenzake.”

SURA YA 3

a Yer 23:3

b Yer 23:4
Eze 34:23

c Ho 1:10

d Zb 87:3
Eze 43:7e Isa 2:2, 3
Isa 56:6, 7
Isa 60:3
Mik 4:1, 2
Zek 2:11
Zek 8:22, 23f Yer 50:4
Eze 37:19
Ho 1:11g 2Nya 36:23
Ezr 1:3
Amo 9:15

h Eze 20:6

i Isa 48:8
Ho 3:1
Ho 5:7j Isa 17:10
Ho 8:14
Ho 13:6

Safu ya 2

a Ho 14:1, 4

b Yer 31:18
Ho 3:5

c Isa 65:7

d Isa 12:2

e Ho 9:10

f Yer 2:19

g Ezr 9:7
Zb 106:7

SURA YA 4

h Yer 3:22
Yoe 2:12, 13

22 “Rudini, ninyi wana waasi. Nitaiponya hali yenu ya uasi.”^a

“Tupo hapa! Tumekuja kwako,

Kwa maana wewe, Ee Yehova, ni Mungu wetu.^b

23 Kwa kweli vilima na machafuko juu ya milima ni udanganyifu.^c

Kwa kweli wokovu wa Israeli uko kwa Yehova Mungu wetu.^d

24 Lakini jambo la aibu li-mekula* kazi ngumu ya mababu zetu tangu ujana wetu,^e

Makundi yao na mifugo yao,

Wana wao na mabinti wao.

25 Na tulale chini katika aibu yetu,

Fedheha yetu na itufunike, Kwa maana tumemtemdea dhambi Yehova Mungu wetu,^f

Sisi na baba zetu tangu ujana wetu mpaka leo hii,^g

Nasi hatujaitii sauti ya Yehova Mungu wetu.”

4 “Ukirudi, Ee Israeli,” asema Yehova,

“Ukirudi kwangu

Na ukiondoa sanamu zako zenye kuchukiza kutoka mbele zangu,

Basi hutakuwa mkimbizi.^h

2 Nawe ukiapa,

‘Kwa hakika kama Yehova anavyoishi!’ katika kweli, haki, na uadilifu,

Ndipo mataifa yatakapojipatia baraka kupitia yeye,

3:24 *Au “mungu wa aibu amekula.”

Nayo yatajigamba kwa sababu yake.”^a

3 Kwa maana Yehova ana-waambia hivi watu wa Yuda na Yerusalemu:

“Jilimieni shamba linalofaa kwa kilimo, Nanyi msieledele kupanda kati ya miiba.”^b

4 Jitahirini kwa ajili ya Yehova,
Na kuondoa magovi ya mioyo yenu,^c
Ninyi watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu,
Ili ghadhabu yangu isiwa-ke kama moto
Na iteketeze bila yeyote wa kuizima,
Kwa sababu ya matendo yenu maovu.”^d

5 Tangazeni jambo hilo Yuda, na kulihubiri Yerusalemu.
Pazeni sauti na kupiga pembe katika nchi yote.^e

Iteni kwa sauti na kusema: “Kusanyikeni pamoja, Nasi tukimbilie katika majiji yenye ngome.”^f

6 Inueni ishara* kuelekea Sayuni.
Tafuteni kimbilio, na msimame tuli,”
Kwa maana ninaleta msiba kutoka kaskazini,^g kishindo kikubwa.

7 Ametokea kama simba kutoka kwenye kichaka chake;^h

Yule anayeyaangamiza mataifa ametoka.ⁱ
Ametoka mahali pake ili kuifanya nchi yako kuwa kitu cha kutisha.

Majiji yako yatakuwa magofu, bila mkaaji.^j

SURA YA 4

a Isa 65:16

b Ho 10:12

c Yer 9:25, 26

d Omb 4:11

e Yer 6:1

f Yer 35:11

g Yer 1:14
Yer 21:7
Yer 25:9

h 2Fa 24:1
2Fa 25:1
Yer 5:6
Yer 50:17

i Eze 26:7

j Isa 5:9
Isa 6:11
Yer 2:15
Yer 9:11

Safu ya 2

a Yer 6:26

b 2Fa 25:5

c Isa 29:9, 10

d Eze 14:9

e Yer 6:13, 14
Yer 14:13
Yer 23:16, 17

f Isa 5:26, 28

8 Kwa hiyo, vaeni nguo za magunia,^a
Ombolezeni* na kupiga mayowe,

Kwa sababu hasira ya Yehova inayowaka hai-jaondoka juu yetu.

9 “Siku hiyo,” asema Yehova, “mfalme atakufa moyo,”^b

Pia wakuu watakufa moyo,^c

Makuhani watashikwa na hofu, nao manabii wata-shangaa.”^c

10 Kisha nikasema: “Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Kwa kweli umewadanganya kabisa watu hawa^d na Yerusalemu, kwa kusema, ‘Mtakuwa na amani,’^e wakati upanga uko kwenye koo zetu.”^f

11 Wakati huo watu hawa na Yerusalemu wataambiwa:

“Upepo unaokausha kuto-ka kwenye vilima vitupu vya jangwani

Utavuma juu ya binti ya* watu wangu;

Hauji kupepeti wala kusa-fisha.

12 Upepo unaovuma kwa nguvu zote unatoka sehemu hizo kwa amri yangu.

Sasa nitatangaza hukumu dhidi yao.

13 Tazameni! Atakuja kama mawingu ya mvua,
Na magari yake ni kama upepo wa dhoruba.^f

4:8 *Au “Pigeni vifua vyenu.” **4:9** *Au “atakosa ujasiri.” #Au “watako-sa ujasiri.” **4:10** *Au “upanga umefikia nafsi zetu.” **4:11** *Tashihisi ya kishai-ri, ambayo labda inaonyesha sikitiko au huruma.

4:6 *Au “nguzo ya ishara.”

Farasi wake wanakimbia
kwa kasi kuliko tai.^a
Ole wetu, kwa sababu tu-
meangamia!

- 14** Usafishe moyo wako uwe
safi kutokana na uovu,
Ee Yerusalemu, ili uoko-
lewe.^b

Utafikiria mambo maovu
mpaka lini?

- 15** Kwa maana sauti inaleta
habari kutoka Dani,^c
Nayo inatangaza msiba ku-
toka kwenye milima ya
Efraimu.

- 16** Tangazeni jambo hilo,
naam, kwa mataifa;
Litangazeni dhidi ya Yeru-
salemu.”

“Walinzi* wanakuja kuto-
ka nchi ya mbali,
Nao watapaza sauti zao
dhidi ya majiji ya Yuda.

- 17** Wanamshambulia kutoka
pande zote kama walinzi
wa shamba ambalo hali-
jazingirwa na ukuta,^d

Kwa sababu ameniasi,^e
asema Yehova.

- 18** “Njia zako mwenyewe na
matendo yako yataletwa
juu yako.^f

Jinsi msiba wako ulivyo
mchungu,

Kwa maana umefika mpa-
ka moyoni mwako!”

- 19** Jamani maumivu yangu,*
maumivu yangu!

Ninahisi uchungu mwingi
moyoni mwangu.^g

Moyo wangu unapigapiga
ndani yangu.

Siwezi kunyamaza,

4:16 *Yaani, wale wanaolitazama jiji
ili wajue wakati wa kushambulia. **4:19**
*Tnn., “matumbo yangu.” #Tnn., “kati-
ka kuta za moyo wangu.”

SURA YA 4

a Kum 28:49, 50
Omb 4:19
Hab 1:8

b Isa 1:16
Eze 18:31

c Yer 8:16

d 2Fa 25:1, 2

e Isa 63:10
Eze 2:3

f Zb 107:17

Safu ya 2

a Sef 1:15, 16

b Yer 10:20

c Yer 6:1

d Kum 32:6
Yer 5:21

e Yer 9:10

f Isa 5:30
Yoe 2:31

g Isa 5:25

h Sef 1:3

i Kum 29:22, 23

Kwa maana nimesikia*
sauti ya pembe,
King'ora cha vita.^{#a}

- 20** Msiba baada ya msiba
umetangazwa,

Kwa maana nchi yote ime-
haribiwa.

Kwa ghafla, mahema
yangu mwenyewe yame-
haribiwa,

Kwa muda mfupi, vita-
mbaa vya mahema
yangu.^b

- 21** Nitaendelea kuona ishara*
mpaka lini,

Na kuendelea kusikia sauti
ya pembe?^c

- 22** Kwa maana watu wangu ni
wajinga;^d

Hawanitambui.

Wao ni wana wapumbavu,
wasio na uelewaji.

Ni werevu* sana katika ku-
tenda maovu,

Lakini hawajui kutenda
mema.

- 23** Niliiona nchi, na tazama!
ilikuwa tupu na ukiwa.^e

Nilitazama mbingu, na
nuru yake haikuwepo.^f

- 24** Niliiona milima, na taza-
ma! ilikuwa ikitetemeka,

Na vilima vilikuwa vikitiki-
sika.^g

- 25** Niliona, na tazama! hapa-
kuwa na mtu yeyote,

Na ndege wote wa angani
walikuwa wamekimbia.^h

- 26** Niliona, na tazama! sasa
shamba la matunda lili-
kuwa nyika,

Na majiji yake yote yaliku-
wa yamebomolewa.ⁱ

4:19 *Au “nafsi yangu imesikia.” #Au
labda, “sauti ya kelele za vita.”
4:21 *Au “nguzo ya ishara.” **4:22** *Au
“Wana hekima.”

Ilikuwa kwa sababu ya Yehova,
Kwa sababu ya hasira yake inayowaka.

- 27** Kwa maana Yehova ana-sema hivi: “Nchi yote itaachwa ukiwa,^a Lakini sitaiangamiza kabisa.
- 28** Kwa sababu hiyo nchi itaomboleza,^b Na juu mbingu zitakuwa na giza.^c Ni kwa sababu nimesema, nami nimeamua, Nami sitabadili nia yangu,* wala sitaliacha jambo hilo.^d
- 29** Kwa sababu ya sauti ya wapanda farasi na wapiga-mishale, Jiji zima linakimbia.^e Wanaingia vichakani, Nao wanapanda kwenye miamba.^f Kila jiji linaachwa, Na hakuna mtu anayeishi humo.”
- 30** Sasa kwa kuwa umeangamizwa, utafanya nini? Ulikuwa ukivaa nguo nyekundu, Ukijipamba kwa mapambo ya dhahabu, Na kupanua macho yako kwa kuyapaka rangi nyeusi.* Lakini ulijirembesha bure,^g Kwa maana waliokutamani wamekukataa; Sasa wanataka kukuua.^h
- 31** Kwa maana nimesikia sauti kama ya mwanamke mgonjwa,

4:28 *Au “sitaghairi.” 4:30 *Au “wanja.”

SURA YA 4

a Law 26:32
2Nya 36:20, 21
Isa 6:11
Yer 10:22
Eze 33:28

b Isa 24:4
Yoe 1:10

c Isa 5:30
Yoe 2:30, 31

d 2Fa 23:26
Eze 24:14

e 2Fa 25:4

f Isa 2:19

g Eze 23:22, 26

h Omb 1:2

Safu ya 2

a Omb 1:17

SURA YA 5

b Eze 22:29
Mik 7:2

c Isa 48:1

d 2Nya 16:9

e 2Nya 28:20-22
Yer 2:30

f Zek 7:11

g Zb 50:17
Isa 42:24, 25
Eze 3:7
Sef 3:2

Maumivu kama ya mwanamke anayezaa mtoto wake wa kwanza,
Sauti ya binti ya Sayuni ambaye anaendelea kuhemahema kwa nguvu. Anasema hivi akiinyoosha mikono yake:^a “Ole wangu, kwa maana nimechoka* kwa sababu ya wauaji!”

- 5** Tembeeni huku na huku katika barabara za Yerusalemu. Tazameni pande zote mwone. Tafuteni katika viwanja vyake vya jiji Ikiwa mnaweza kumpata mtu anayetenda haki,^b Yeyote anayejitahidi kuwa mwaminifu, Nami nitalisamehe jiji hilo.
- 2** Hata wakisema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi!” Bado wataapa kwa uwongo.^c
- 3** Ee Yehova, je, macho yako hayatafuti uaminifu?^d Uliwapiga, lakini hawakusikia.* Uliwaangamiza, lakini walikataa kukubali nidhamu.^e Walizifanya nyuso zao kuwa ngumu kuliko mwamba,^f Nao wakakataa kugeuka.^g
- 4** Lakini nilisema moyoni: “Kwa hakika hawa ni watu wa hali ya chini. Wanatenda kwa upumbavu, kwa sababu hawajui njia ya Yehova, Hukumu ya Mungu wao.

4:31 *Au “nafsi yangu imechoka.” 5:3 *Tnn., “hawakudhoofika.”

16 Podo lao ni kama kaburi lililo wazi;
Wote ni mashujaa.

17 Watakula mavuno yenu na mkate wenu.^a

Watawala wana wenu na mabinti wenu.

Watajala makundi yenu na mifugo yenu.

Wataila mizabibu yenu na mitini yenu.

Watayaangamiza kwa upanga majiji yenu yenye ngome mnyoyatu-maini.”

18 “Lakini hata katika siku hizo,” asema Yehova, “sita-waangamiza kabisa.^b **19** Na wakiuliza, ‘Kwa nini Yehova Mungu wetu ametutenda mambo haya yote?’ mtawajibu, ‘Kama mlivyoniacha ili kumtumikia mungu wa kigeni katika nchi yenu, ndivyo mtakavyowatumikia wageni katika nchi isiyoyenu.’”^c

20 Tangazeni jambo hili katika nyumba ya Yakobo, Na kulitangaza Yuda, mki-sema:

21 “Sikieni jambo hili, ninyi watu wajinga na wasio na akili:^{*d}

Wana macho lakini hawa-
wezi kuona;^e

Wana masikio lakini hawa-
wezi kusikia.^f

22 ‘Je, hamniogopi mimi?’
asema Yehova,

‘Je, hampaswi kutetemeka
mbele zangu?’

Mimi ndiye niliyeweka
mchanga kuwa mpaka
wa bahari,

Sheria inayodumu isiyowe-
za kukiukwa na bahari.

5:21 *Tnn., “ninyi watu wajinga msio na moyo.”

SURA YA 5

a Law 26:16

b Yer 4:27

c Kum 4:27
Kum 28:48
Kum 29:24, 25
2Nya 7:21, 22

d Yer 4:22

e Isa 59:10

f Isa 6:9
Eze 12:2
Mt 13:13

Safu ya 2

a Ayu 38:8, 11
Zb 33:7
Met 8:29

b Zb 95:10
Yer 11:8

c Kum 11:14

d Kum 28:23, 24
Yer 3:3

e Amo 8:5
Mik 6:11, 12

f Isa 1:23

g Zb 82:2

Ingawa mawimbi yake
yanasukasuka, hayawezi
kushinda;

Ingawa yananguruma,
bado hayawezi kuvuka.^a

23 Lakini watu hawa wana moyo mgumu unaoasi;
Wamegeuka kando na kuiu-
fuata njia yao wenyewe.^b

24 Nao hawasemi moyoni
mwao:

“Sasa na tumwogope Ye-
hova Mungu wetu,

Yule anayeleta mvua kati-
ka majira yake,

Mvua ya vuli na mvua ya
masika,

Yule anayetulindia ma-
juma yaliyowekwa ya
mavuno.”^c

25 Makosa yenu wenyewe
yalizuia mambo haya
yasije;

Dhambi zenu wenyewe
zimewanyima mambo
mema.^d

26 Kwa maana kati ya watu
wangu kuna watu waovu.
Wanaendelea kuchungulia,
kama wawindaji wa nde-
ge wanapochutama.

Wanatega mtego hatari.
Wanawanasa watu.

27 Kama kizimba kilichojaa
ndege,
Ndivyo nyumba zao zili-
vyojaa udanganyifu.^e

Ndiyo sababu wamekuwa
wenye nguvu na matajiri.

28 Wamenenepa na kuwa
laini;

Wanafurika uovu.

Hawateteti mayatima ka-
tika kesi,^f

Wanatafuta mafanikio yao
wenyewe;

Nao wanawanyima haki
maskini.”^g

- 29** “Je, sipaswi kuwafanya wawajibike kwa sababu ya mambo haya,” asema Yehova.
 “Je, sipaswi* kujilipizia kisasi dhidi ya taifa kama hili?”
- 30** Jambo la kutisha na kuchukiza limetokea nchini:
- 31** Manabii wanatabiri uwo-ngo,^a
 Nao makuhani wanakanda-
 miza kwa mamlaka yao wenyewe.
 Na watu wangu wanape-
 nda mambo yawe hivyo.^b
 Lakini mtafanya nini mwi-
 sho ukifika?”
- 6** Kimbilieni usalama, enyi wana wa Benjamini, mbali na Yerusalemu. Pigeni pembe^c huko Te-koa;^d
 Washeni ishara ya moto Beth-hakeremu!
 Kwa maana msiba unakuja kutoka kaskazini, msiba mkubwa.^e
- 2** Binti ya Sayuni anafanana na mwanamke mrembo na mwororo.^f
- 3** Wachungaji watakuja na mifugo yao.
 Watapiga mahema yao kumzunguka pande zote,^g
 Kila mmoja akilisha mifugo anayotunza.^h
- 4** “Jitayarisheni kupigana vita naye!”
 Simameni, tumshambulie wakati wa aduhuri!”
 “Ole wetu, kwa maana siku inakwisha,
 Kwa maana vivuli vya jioni vinarefuka!”

5:29 *Au “nafsi yangu haipaswi.” 6:4 *Tnn., “Takaseni vita dhidi yake.”

SURA YA 5

a Yer 14:14
 Omb 2:14
 Eze 13:6

b Isa 30:10
 Yoh 3:19

SURA YA 6

c Yer 4:5

d 2Nya 11:5, 6
 Amo 1:1

e Yer 1:14
 Yer 10:22

f Isa 3:16

g 2Fa 25:1

h Yer 4:16, 17

Safu ya 2

a 2Nya 36:17, 19
 Amo 2:5

b Eze 21:21, 22

c 2Fa 21:16
 Eze 7:23

d Eze 7:11
 Mik 2:2

e Eze 23:18

f Law 26:34
 Yer 9:11

g Isa 6:10
 Mdo 7:51

- 5** “Simameni, tumshambulie usiku
 Na kuiharibu minara yake yenye ngome.”^a
- 6** Kwa maana Yehova wa majeshi anasema hivi:
 “Kateni miti na mjenge boma la kuzingira Yerusalemu.^b
 Yeye ni jiji ambalo lazima liadhibiwe;*
 Hamna lolote ndani yake isipokuwa ukandamizaji.^c
- 7** Kama tangi linavyohifadhi maji yake yakiwa baridi, Ndivyo anavyohifadhi uovu wake ukiwa baridi. Ukatili na maangamizi yanasikiwa ndani yake;^d
 Ugonjwa na tauni viko mbele zangu daima.
- 8** Nakuonya, Ee Yerusalemu, la sivyo nitakuacha* kwa chuki;^e
 Nitakufanya uwe ukiwa, nchi isiyo na wakaaji.”^f
- 9** Yehova wa majeshi anasema hivi:
 “Watawaokota kikamilifu Waisraeli watakaobaki kama zabibu za mwisho zilizo kwenye mzabibu. Pitisha mkono wako tena kama mtu anayekusanya zabibu kwenye miza-bibu.”
- 10** “Nitazungumza na nani na kumwonya?
 Ni nani atakayesikiliza? Tazama! Masikio yao yamezibwa* hivi kwamba hawawezi kusikiliza.^g
 Tazama! Neno la Yehova

6:6 *Au “liwajibishwe.” 6:8 *Au “nafsi yangu itakuacha.” 6:10 *Tnn., “Sikio lao halijatahiriwa.”

limekuwa kitu wanachokidharau;^a

Hawapendezwi nalo.

- 11** Basi nimejawa na ghadhabu ya Yehova,

Nami nimechoka kuizuia ndani yangu.”^b

“Imwage juu ya mtoto aliye barabarani,^c

Juu ya vikundi vya vijana waliokusanyika pamoja.

Wote watakatwa, mwanamume pamoja na mke wake,

Wazee pamoja na waliozeeka sana.”^d

- 12** Watu wengine watapewa nyumba zao,

Pamoja na mashamba yao na wake zao.”^e

Kwa maana nitaunyoosha mkono wangu dhidi ya wakaaji wa nchi,” asema Yehova.

- 13** “Kwa maana kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi, kila mmoja anajipatia faida isiyu ya haki;^f

Kuanzia nabii mpaka kuhani, kila mmoja anaitenda kwa ulaghai.”^g

- 14** Nao wanajaribu kuponya kijuujuu jeraha* la watu wangu, wakisema,

‘Kuna amani! Kuna amani!’ Wakati hakuna amani.”^h

- 15** Je, wanaona aibu kwa sababu ya mambo yanayochukiza waliyotenda?

Hawaoni aibu hata kidogo! Hata hawajui jinsi ya kufedheheka!ⁱ

Basi wataanguka miongoni mwa wale walioanguka.

Nitakapowaadhibu watajiki kwa,” asema Yehova.

6:11 *Tnn., “wale waliojaa siku.” 6:14

*Au “jeraha la kuvunjika.”

SURA YA 6

a 2Nya 36:15, 16
Yer 20:8

b Yer 20:9

c Yer 18:21

d Eze 9:6

e Kum 28:30
Yer 8:10
Omb 5:11
Sef 1:13

f Eze 22:12

g Yer 2:8
Yer 8:10-12
Yer 23:11
Mik 3:5, 11
Sef 3:4

h Yer 14:13
Yer 23:16, 17
Eze 13:10
1Th 5:3

i Yer 3:3

Safu ya 2

a Isa 30:21

b Yer 18:15

c Yer 25:4
Eze 3:17
Hab 2:1

d Isa 58:1

e Zek 7:11

f Kum 4:25, 26
Da 9:12

g Isa 1:11
Isa 66:3
Yer 7:21
Amo 5:21

- 16** Yehova anasema hivi:

“Simameni kwenye makutano ya barabara mwone.

Ulizeni kuhusu barabara za zamani za kale,

Ulizeni mahali ilipo njia nzuri, nanyi mtembee ndani yake,”^a

Nanyi mtajipumzisha.”* Lakini wanasema: “Hatutatembea kwenye njia hiyo.”^b

- 17** “Nami nikawaweka walinzi^c waliosema, ‘Isikilizeni sauti ya pembe!’”^d

Lakini wakasema: “Hatutaisikiliza.”^e

- 18** “Kwa hiyo sikieni, enyi mataifa!

Nawe ujue, Ee kusanyiko, Jambo litakalowapata.

- 19** Sikiliza, Ee dunia! Ninawaitea msiba watu hawa^f

Kama matunda ya mipango yao,

Kwa maana hawakuyasiliza maneno yangu

Nao waliikataa sheria* yangu.”

- 20** “Ninafaidikaje mnapoleta ubani kutoka Sheba

Na utete wenye manukato kutoka nchi ya mbali?

Dhabihu zenu nzima za kuteketezwa hazikubaliki,

Na dhabihu zenu hazinipe ndezi.”^g

- 21** Kwa hiyo Yehova anasema hivi:

“Ninawawekea watu hawa vikwazo,

Nao watajikwaa juu yake, Akina baba na wana pia,

6:16 *Au “mtajipumzisha nafsi zenu.”

6:19 *Au “waliyakataa mafundisho.”

Jirani na mwenzake,
Nao wataangamia wote.”^a

22 Yehova anasema hivi:
“Tazama! Watu wanakuja
kutoka nchi ya kaskazini,
Na taifa kubwa litaa-
mshwa kutoka sehemu
za mbali zaidi za dunia.”^b

23 Watashika upinde na
mkuki.
Ni wakatili na hawatakuwa
na huruma.
Sauti yao itanguruma
kama bahari,
Nao wanapanda farasi.^c
Wanajipanga kivita dhidi
yako kama mwanamume
wa vita, Ee binti ya Sa-
yuni.”

24 Tumesikia habari zake.
Mikono yetu imelegea.^d
Taabu imetushika,
Maumivu kama ya* mwa-
namke anayezaa.^e

25 Usiende shambani,
Wala usitembee baraba-
rani,
Kwa maana adui ana upa-
nga;
Kuna hofu kila upande.

26 Ee binti ya watu wangu,
Vaa nguo za magunia^f na
ugaegae katika majivu.
Omboleza kana kwamba
unamwombolezea mwa-
na wa pekee, kwa kilio
cha uchungu,^g

Kwa maana mwangamizaji
atatushambulia kwa
ghafila.^h

27 “Nimekufanya wewe*
kuwa mpimaji wa madini
miongoni mwa watu
wangu,
Mtu anayefanya uchunguzi
kamili;

6:24 *Tnn., “Uchungu wa kuzaa kama
wa.” 6:27 *Yaani, Yeremia.

SURA YA 6

a 2Nya 36:17
Omb 2:21

b Yer 1:14
Yer 25:9

c Hab 1:8

d Eze 21:7

e Yer 4:31

f Yer 4:8

g Omb 1:2, 16

h Yer 15:8

Safu ya 2

a Isa 30:1
Isa 48:4
Yer 5:23

b Yer 9:4

c Yer 9:7
Eze 22:20

d Eze 24:13

e Yer 14:19
Omb 5:22

SURA YA 7

f Yer 26:13

g Mik 3:11

h Yer 21:12
Yer 22:3

Unapaswa kuangalia na
kuchunguza njia yao.

28 Wote ni watu wakaidi
kabisa,^a
Wanaotembea huku na
huku wakichongea.^b
Wao ni kama shaba na
chuma;

Wote wamepotoka.

29 Vifaa vya kuvukuta vi-
meunguzwa.
Risasi inatoka kwenye
moto wao.

Mtu anaendelea kuwasafi-
sha sana lakini anafanya
kazi ya bure,^c

Na wale wabaya hawajate-
ngwa.^d

30 Hakika watu watawaita fe-
dha iliyokataliwa,
Kwa maana Yehova ame-
wakataa.”^e

7 Hili ndilo neno lililomjia
Yeremia kutoka kwa Yeho-
va, likisema: **2** “Simama ka-
tika lango la nyumba ya Yeho-
va nawe utangaze hapo ujumbe
huu, ‘Sikieni neno la Yeho-
va ninyi watu wote wa
Yuda mnaingia katika mala-
ngo haya ili kumwinamia
Yehova. **3** Yehova wa maje-
shi, Mungu wa Israeli, anase-
ma hivi: “Rekebisheni njia
zenu na matendo yenu, nami
nitawaruhusu mwendelee ku-
kaa mahali hapa.”^f **4** Msiya-
tumaini maneno ya udangan-
yifu na kusema, ‘Hili ni* he-
kalu la Yehova, hekalu la Ye-
hova, hekalu la Yehova!’^g **5** M-
kirekebisha kikweli njia
zenu na matendo yenu; mki-
tekeleza haki kikweli kati ya
mtu na jirani yake;”^h **6** msipo-
wakandamiza wakaaji wageni,

7:4 *Tnn., “Haya ni,” yaani majengo yote
ya hekalu.

mayatima,* na wajane;^a msipomwaga damu isiyu na hatia mahali hapa; na msipoifuata miungu mingine na kujiletea madhara;^b **7** basi nitawaruhusu mwendelee kukaa mahali hapa, katika nchi niliyowapa mababu zenu daima.”””*

8 “Lakini mnayatumaini maneno ya udanganyifu^c—hatawaletea faida yoyote. **9** Je, mnaweza kuiba,^d kuua, kufanya uzinzi, kuapa kwa uwongo,^e kumtolea dhabihu* Baali,^f na kuifuata miungu mingine ambayo hamkuijua, **10** kisha mje na kusimama mbele zangu katika nyumba hii inayoitwa kwa jina langu na kusema, ‘Tutaokolewa,’ ilhali mnafanya mambo hayo yote yanayochukiza? **11** Je, nyumba hii inayoitwa kwa jina langu imekuwa pango la wanyang’anyi machoni penu?^g Nimejionea jambo hilo,” asema Yehova.

12 “Hata hivyo, sasa nendeni mahali pangu huko Shilo,^h ambapo mwanzoni nilifanya jina langu likae,ⁱ na kuona nilivyopafanya kwa sababu ya uovu wa watu wangu Waisraeli./ **13** Lakini mliendelea kufanya mambo hayo yote,’ asema Yehova, ‘na ingawa nilizungumza nanyi tena na tena,* hamkusikiliza.^k Niliendelea kuwaita, lakini hamkujibu./ **14** Ndivyo nitakavyoitendea nyumba inayoitwa kwa jina langu,^m ambayo mnaitumaini,ⁿ na mahali hapa ambapo niliwapa ninyi na mababu zenu, kama nilivyoitendea Shilo.^o **15** Nitawatupa kutoka mbe-

7:6 *Au “watoto wasio na baba.” **7:7** *Au “tangu milele mpaka milele.” **7:9** *Au “moshi wa dhabihu.” **7:13** *Tnn., “niliamka mapema na kuzungumza.”

SURA YA 7

a Kum 24:17
Zb 82:3
Zek 7:9, 10
Yak 1:27

b Kum 8:19

c Isa 30:10
Yer 5:31
Yer 14:14

d Isa 3:14
Mik 2:2

e Yer 5:2

f Yer 11:13

g Mt 21:13
Mk 11:17
Lu 19:45, 46

h Yos 18:1

i Kum 12:5, 11

j 1Sa 4:11
Zb 78:60
Yer 26:6, 9

k 2Nya 36:15, 16
Yer 25:3, 4

l Isa 65:12

m 2Fa 25:8, 9

n Yer 7:4

o 1Sa 4:10, 11
Zb 78:60
Yer 26:4, 6
Omb 2:7

Safu ya 2

a 2Fa 17:22, 23

b Kut 32:9, 10
Yer 11:14

c Yer 15:1

d Yer 44:17

e Isa 57:6
Yer 19:13
Eze 20:28

f Da 9:7

g Omb 2:3

h 2Fa 22:17
Yer 17:27

i Isa 1:11
Yer 6:20
Ho 8:13
Amo 5:21

j 1Sa 15:22
Ho 6:6

le za macho yangu, kama nilivyowatupa ndugu zenu wote, wazao wote wa Efraimu.’^a

16 “Lakini wewe, usisali kwa ajili ya watu hawa. Usipaze kilio wala kusali wala kuni-sihi kwa ajili yao,^b kwa maana sitakusikiliza.^c **17** Je, huoni mambo wanayofanya katika majiji ya Yuda na kwenye barabara za Yerusalemu? **18** Wana wanakusanya kuni, akina baba wanawasha moto, na wake wanakanda unga ili kumwokea Malkia wa Mbinguni*^d keki za dhabihu, nao wanaimiminia miungu mingine matoleo ya kinywaji ili wanikasirishe.^e **19** ‘Lakini je, ni mimi wanayeniumiza?’* auliza Yehova. ‘Je, hawajiumizi wao wenyewe, kwa aibu yao wenyewe?’^f **20** Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema, ‘Tazama! Hasira yangu na ghadhabu yangu zitamwagwa mahali hapa,^g juu ya mwanadamu na mnyama, juu ya miti ya shambani na mazao ya ardhi; itateketeza na haitazimwa.’^h

21 “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema, ‘Endeleeni, ongezeni dhabihu zenu nzima za kuteketezwa kwenye dhabihu zenu nyingine, na mle nyama hizo ninyi wenyewe.’ⁱ **22** Kwa maana siku niliyowatoa mababu zenu nchini Misri, sikuwaambia wala kuwaamuru kuhusu dhabihu nzima za kuteketezwa na dhabihu nyingine./ **23** Lakini niliwaamuru hivi: “Tiini sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi

7:18 *Jina la mungu wa kike aliyeabudiwa na Waisraeli waasi imani; huenda ni mungu wa kike wa uzazi. **7:19** *Au “wanayenikasirisha; wanayenichokoza.”

mtakuwa watu wangu.^a Ni lazima mtembee katika njia yote ninayowaamuru, ili mambo yawaendee vema.”^b **24** Lakini hawakusikiliza wala kute-ga sikio lao;^c badala yake walitembea katika mipango yao* wenyewe, wakifuata kwa ukaidi moyo wao mwovu,^d nao wakarudi nyuma, badala ya kwenda mbele, **25** tangu siku ambayo mababu zenu walitoka nchini Misri mpaka leo hii.^e Basi nikaendelea kuwatuma kwenu watumishi wangu wote manabii, nilikuwa nikiwatuma kila siku, tena na tena.*^f **26** Lakini walikataa kunisikiliza, nao hawakutega sikio lao.^g Badala yake, walikuwa wakaidi,* nao walitenda mambo mabaya zaidi kuliko mababu zao!

27 “Utawaambia maneno haya yote,^h lakini hawatakusikiliza; utawaaita, lakini hawatakujibu. **28** Nawe utawaambia, ‘Hili ndilo taifa ambalo halikuitii sauti ya Yehova Mungu wao, nao walikataa kukubali nidhamu. Uaminifu ume-toweka na hata hautajwi miongoni mwao.’ⁱ

29 “Nyoa nywele zako ambazo hazijanyolewa,* nawe uzitupe, na uimbe wimbo wa huzuni[†] juu ya vilima vitupu, kwa maana Yehova amekikataa na atakiacha kizazi hiki ambacho kimemkasirisha. **30** ‘Kwa maana watu wa Yuda wametenda maovu machoni pangu,’ asema Yehova. ‘Wameziweka sanamu zao zinazo-

7:24 *Au “ushauri wao.” 7:25 *Tnn., “kila siku niliamka mapema na kuwatumama.” 7:26 *Tnn., “waliifanya shingo yao iwe ngumu.” 7:28 *Tnn., “umekata kutoka kinywani mwao.” 7:29 *Au “ambazo zimewekwa wakfu.” †Au “wimbo wa maimbalezo.”

SURA YA 7

a Kut 19:5
Law 26:3, 12

b Kum 5:29

c Kut 32:8

d Ho 4:16
Zek 7:12e Kum 9:7
Isa 8:8f 2Fa 17:13
2Nya 36:15
Ne 9:17, 30
Yer 25:4g 2Nya 33:10
Yer 25:3h Yer 26:2
Eze 2:7i Yer 5:1
Mik 7:2

Safu ya 2

a 2Fa 21:1, 4
2Nya 33:1, 4
Yer 23:11
Yer 32:34

b Yos 15:8, 12

c Kum 12:29-31
2Fa 17:17
2Nya 28:1, 3
2Nya 33:1, 6
Eze 20:31d Law 18:21
Law 20:3
Yer 19:5, 6
Yer 32:35e Yer 19:11
Eze 6:4, 5f Kum 28:26
Zb 79:2
Yer 16:4g Isa 24:8
Yer 25:10h Law 26:33
Isa 1:7
Isa 6:11

SURA YA 8

i Kum 4:19
2Fa 17:16
2Fa 21:1, 3
Yer 19:13
Eze 8:16
Sef 1:4, 5

j Yer 16:4

chukiza katika nyumba ambayo imeitwa kwa jina langu, ili kuitia unajisi.^a **31** Wamejenga mahali pa juu pa Tofethi, palipo katika Bonde la Mwana wa Hinomu,^{*b} ili kuwateketeza motoni wana wao na mabinti wao,^c jambo ambalo sikuumuru na ambalo hata halijawahi kamwe kuingia moyoni mwangu.’^{†d}

32 “Kwa hiyo tazama! siku zinakuja,’ asema Yehova, ‘wakati ambapo bonde hilo halitaitwa tena Tofethi au Bonde la Mwana wa Hinomu* bali Bonde la Mauaji. Watawazika wafu katika Tofethi hivi kwamba hakutakuwa na nafasi zaidi.^e **33** Na maiti za watu hawa zitakuwa chakula cha ndege wa angani na cha wanyama wa duniani, na hakuna mtu atakayewafukuza.^f **34** Nitaikomesha sauti ya furaha na sauti ya shangwe, sauti ya bwana harusi na sauti ya bibi harusi,^g katika majiji ya Yuda na katika barabara za Yerusalemu, kwa maana nchi itakuwa magofu.’^h

8 “Wakati huo,” asema Yehova, “mifupa ya wafalme wa Yuda, mifupa ya wakuu wake, mifupa ya makuhanani, mifupa ya manabii, na mifupa ya wakaaji wa Yerusalemu itatolewa katika makaburi yao. **2** Itatandazwa juani na mbele ya mwezi na kwa jeshi lote la mbinguni ambalo wamelipenda na kulitumikia na kulifuata na kulitafuta na kuliinamia.ⁱ Haitakusanywa, wala haitazikwa. Itakuwa kama mbolea juu ya ardhi.’^j

7:31, 32 *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Gehena.” 7:31 #Au “sijawahi kamwe kulifikiria.”

3 “Na wale watakaobaki na kuokoka wa familia hii yenye uovu watachagua kifo bada-la ya uhai katika sehemu zote ambazo nitawatawanya,” asema Yehova wa majeshi.

4 “Nawe unapaswa kuwaambia, ‘Yehova anasema hivi:

“Je, wataanguka na wasisi-mame tena?

Mtu akigeuka, je, yule mwingine hatageuka pia?

5 Kwa nini watu hawa, Yerusalemu, wanakosa uaminifu kwa ukosefu wa uaminifu unaodumu?

Wanashika kwa nguvu udanganyifu;

Wanakataa kugeuka.^a

6 Nilitega sikio na kuendelea kusikiliza, lakini mazungumzo yao hayakuwa mazuri.

Hakuna mtu aliyetubu uovu wake au kuuliza, ‘Nimefanya nini?’^b

Kila mmoja anarudi tena na tena kwenye njia inayopendwa na wengi, kama farasi anayekimbia kasi kuingia vitani.

7 Hata korongo angani anajua majira yake;*

Njiwa tetere na mbuyu-wayu na teleka[#] hawachelewi kurudi.^Δ

Lakini watu wangu hawaelewi hukumu ya Yehova.”^c

8 ‘Mnawezaje kusema: “Tuna hekima, nasi tuna sheria* ya Yehova”?

Kwa hakika, kalamu ya uwongo^{#d} ya waandi-

8:7 *Au “nyakati zake zilizowekwa.”

[#]Au labda, “korongo.” ^ΔAu “kuhama.”

8:8 *Au “mafundisho.” [#]Au “udanganyifu.”

SURA YA 8

a Yer 5:3

b Yer 5:1

c Isa 1:3

d Isa 8:1

Safu ya 2

a Isa 29:14

b Kum 28:30
Sef 1:13

c Isa 56:11
Eze 33:31
Mik 3:11

d Yer 5:31
Yer 6:12-15
Yer 27:9
Omb 2:14
Eze 22:28

e Yer 23:16, 17
Eze 13:10

f Yer 3:3

g Yer 23:12

shi imetumiwa kuandika uwongo tu.

9 Wenye hekima wameaibishwa.^a

Wameogopa nao watashikwa.

Tazama! Wamelikataa neno la Yehova,

Nao wana hekima gani?

10 Basi nitawapa wanaume wengine wake zao, Na mashamba yao nitawapa wamiliki wengine;^b

Kwa maana kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi, kila mmoja anajipatia faida isiyo ya haki;^c

Kuanzia nabii mpaka kuhani, kila mmoja anaitenda kwa ulaghai.^d

11 Nao wanajaribu kuponya kijuujuu jeraha* la binti ya watu wangu, waki-sema,

“Kuna amani! Kuna amani!”

Wakati hakuna amani.^e

12 Je, wanaona aibu kwa sababu ya mambo yenye kuchukiza waliyotenda? Hawaoni aibu hata kidogo! Hata hawajui jinsi ya kufedheheka!^f

Basi wataanguka kati ya wale walioanguka.

Nitakapowaletea adhabu watajikwaa,^g asema Yehova.

13 ‘Nitakapowakusanya, nitawamaliza,’ asema Yehova.

‘Hakutakuwa na zabibu zitakazobaki kwenye mzabibu, wala tini kwenye mtini, na majani yatanyauka.

8:11 *Au “jeraha la kuvunjika.”

Nao watapoteza kile nili-chowapa.”

- 14 “Kwa nini tunaketi hapa? Tukasanyikeni pamoja tuingie katika majiji yenye ngome^a na kuangamia humo.

Kwa maana Yehova Mungu wetu atatuangamiza, Naye anatupatia maji yenye sumu tunywe,^b

Kwa sababu tumemtendea Yehova dhambi.

- 15 Tulitumaini kupata amani, lakini hakuna jambo lolote jema lililokuja, Wakati wa kuponywa, lakini kuna hofu!^c

- 16 Mikoromo ya farasi wake inasikika kutoka Dani.

Kwa sababu ya mlio wa farasi dume wake,

Nchi nzima inatetemeka. Wanaingia na kuinyafua nchi na kila kitu kili-chomo,

Jiji na wakaaji wake.”

- 17 “Kwa maana ninawatuma nyoka kati yenu, Nyoka wenye sumu wasio-weza kucheza, Nao hakika watawauma,” asema Yehova.

- 18 Huzuni yangu haiwezi kuponywa;

Moyo wangu ni mgonjwa.

- 19 Kutoka nchi ya mbali kuna kilio cha kuomba msaa

Kutoka kwa binti ya watu wangu:

“Je, Yehova hayuko Sayuni?”

Au je, mfalme wake hayuko ndani yake?”

“Kwa nini wamenikasirisha kwa sanamu zao za kuchongwa,

SURA YA 8

a Yer 4:5

b Yer 9:15
Yer 23:15
Omb 3:19

c Yer 4:10
Yer 14:19

Safu ya 2

a Yer 4:19, 20
Yer 14:17

b Mwa 37:25

c Yer 30:12, 13

d Yer 30:17
Yer 33:4, 6

SURA YA 9

e Isa 22:4
Yer 13:17

f Yer 5:7
Yer 23:10

g Isa 59:3

h Yer 4:22

Kwa miungu yao ya kigeni ya ubatili?”

- 20 “Mavuno yamepita, kiangazi kimeisha, Lakini hatujaakolewa!”

- 21 Nimevunjwawunjwa kwa sababu ya jeraha* la binti ya watu wangu;^a Nimehuzunika.

Nimepatwa na mshtuko.

- 22 Je, hakuna zeri* kule Gileadi?^b

Au, je, hakuna mponyaji[#] huko?^c

Kwa nini binti ya watu wangu hajaponywa?^d

- 9 Laiti kichwa changu kingenkuwa maji,

Na macho yangu chemchemi ya machozi!^e

Ndipo ningelia usiku na mchana

Kwa ajili ya watu wangu waliouawa.

- 2 Laiti ningepata mahali ambapo wasafiri hulala nyikani!

Ndipo ningewaacha watu wangu na kwenda mbali nao,

Kwa maana wote ni wazi-nzi,^f

Kundi la watu wenye hila.

- 3 Wanaupinda ulimi wao kama upinde;

Uwongo, badala ya uamini-fu, umeenea nchini.^g

“Wanatoka uovu hadi uovu zaidi,

Nao hawanisikilizi,^h asema Yehova.

- 4 “Kila mtu, jihadhari na jirani yako, Wala usimwamini hata ndugus yako.

8:21 *Au “jeraha la kuvunjika.” 8:22 *Au “mafuta yanayotuliza.” #Au “tabibu.”

Kwa maana kila ndugu ni msaliti,^a
Na kila jirani ni mcho-ngezi.^b

5 Kila mtu anamdanganya jirani yake,
Na hakuna yeyote anaye-sema ukweli.

Wameufundisha ulimi wao kusema uwongo.^c

Wanajichosha kwa kufanya makosa.

6 Unaishi katikati ya udanganyifu.

Katika udanganyifu wao walikataa kunijua mimi," asema Yehova.

7 Kwa hiyo Yehova wa majeshi anasema hivi:
"Nitawayeyusha na kuwajaribu,^d

Kwa maana ni nini kingine ninachoweza kumtendea binti ya watu wangu?"

8 Ulimi wao ni mshale unaoua na kusema udanganyifu.

Kwa kinywa chake mtu anazungumza na jirani yake kuhusu amani, Lakini ndani anamvizia."

9 "Je, sipaswi kuwafanya wawajibike kwa sababu ya mambo haya?" asema Yehova.

"Je, sipaswi* kujilipizia kisasi dhidi ya taifa kama hili?"^e

10 Nitalia na kuiomboleza milima

Na kuimba wimbo wa huzuni* kwa ajili ya mali-sho ya nyikani,
Kwa maana yametekete-

9:9 *Au "nafsi yangu haipaswi." 9:10

*Au "wimbo wa maombolezo."

SURA YA 9

a Yer 12:6
Mik 7:2, 5

b Yer 6:28
Eze 22:9

c Zb 50:19
Mik 6:12

d Isa 1:25
Isa 48:10

e Yer 5:9, 29

Safu ya 2

a Yer 4:25
Sef 1:3

b Zb 79:1
Yer 26:18

c Yer 10:22

d Yer 4:27
Yer 25:11
Yer 32:43

e Yer 7:24

f Amu 3:7
1Sa 12:10
Ho 11:2

g Yer 8:14
Yer 23:15
Omb 3:15, 19

h Law 26:33
Kum 28:64
Zb 106:27
Zek 7:14

i Yer 29:17
Eze 5:2

zwa hivi kwamba hakuna mwanadamu anayepita humo,

Na sauti ya mifugo haisikiwi.

Ndege wa angani na wanyama wamekimbia; wametoweka.^a

11 Nitalifanya Yerusalemu kuwa rundo la mawe,^b mapango ya mbwamwitu,^c

Nami nitayafanya majiji ya Yuda yawe ukiwa, bila mkaaji.^d

12 Ni nani mwenye hekima ya kutosha kuelewa jambo hili?

Kinywa cha Yehova kimezungumza na nani, ili atangaze jambo hilo?

Kwa nini nchi imeangamia?

Kwa nini imeteketewa kama nyika,

Hivi kwamba hakuna mtu anayepita humo?"

13 Yehova akajibu: "Kwa sababu wameikataa sheria* yangu niliyowapa, na kwa sababu hawajaifuata na kutii sauti yangu. **14** Badala yake, walifuata kwa ukaidi mioyo yao wenyewe,^e na kuzifuata sanamu za Baali, kama baba zao walivyowafundisha kufanya.^f **15** Kwa hiyo, Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: "Tazama, ninawafanya watu hawa wale pakanga, nami nitawafanya wanywe maji yenye sumu.^g

16 Nitawatawanya kati ya mataifa ambayo wao na baba zao hawajayajua,^h nami nitatuma upanga uwafuate mpa-ka nitakapowaangamiza kabisa."ⁱ

9:13 *Au "wameyakataa mafundisho."

17 Yehova wa majeshi anasema hivi:

“Tendeni kwa uelewaji.
Waiteni wanawake wanaoimba nyimbo za huzuni,*^a
Nanyi waiteni wanawake stadi waje,

18 Ili waje haraka na kutuombolezea,
Ili macho yetu yabubujike machozi

Na kope zetu zitiririke maji.^b

19 Kwa maana sauti ya maombolezo imesikika kutoka Sayuni:^c

“Jinsi tulivyoangamizwa!
Jinsi aibu yetu ilivyo nyingi!

Kwa maana tumeiacha nchi, nao wamezibomoa nyumba zetu.”^d

20 Enyi wanawake, sikieni neno la Yehova.
Sikio lenu na lipokee neno la kinywa chake.

Wafundisheni mabinti wenu maombolezo haya,
Na mfundishane wimbo huu wa huzuni.*^e

21 Kwa maana kifo kimeingia kupitia madirisha yetu;
Kimeingia ndani ya minara yetu yenye ngome

Ili kuwaondoa watoto barabarani

Na vijana kwenye viwanja vya jiji.’^f

22 Sema, ‘Yehova anasema hivi:

“Maiti za watu zitaanguka kama mbolea juu ya ardh shambani,
Kama safu ya miganda ya nafaka iliyotoka kukatwa na mvunaji,

SURA YA 9

a 2Nya 35:25

b Yer 6:26
Yer 14:17

c Yer 4:31
Eze 7:16
Mik 1:8, 9

d Omb 4:15
Mik 2:10

e Isa 29:2
Yer 7:29

f 2Nya 36:17
Yer 6:11

Safu ya 2

a Isa 5:25
Yer 16:3, 4

b Isa 5:21

c Kum 8:12-14
Kum 8:17, 18

d 1Ko 1:31
2Ko 10:17

e Kut 34:6
Zb 89:14

f Zb 99:4
Ho 6:6
Mik 6:8
Mik 7:18

g Amo 3:1, 2

h Isa 19:1
Eze 29:2

i Isa 1:1

j Yer 27:2, 3
Eze 32:29
Oba 1

k Yer 49:1
Eze 25:2

l Isa 15:1
Yer 48:1

m Yer 25:17, 23
Yer 49:32

n Law 26:41
Yer 4:4

SURA YA 10

o Law 18:3, 30
Law 20:23
Kum 12:30

Bila mtu wa kuikusanya.””^a

23 Yehova anasema hivi:
“Mtu mwenye hekima asijigambe kwa sababu ya hekima yake;^b

Mtu mwenye nguvu asijigambe kwa sababu ya nguvu zake;

Na tajiri asijigambe kwa sababu ya utajiri wake.”^c

24 “Lakini yule anayejigamba na ajigambe* kwa jambo hili:

Kwamba ana ufahamu na ujuzi kunihusu,^d

Kwamba mimi ni Yehova, Ninayetenda kwa upeendo mshikamanifu, haki, na uadilifu duniani.^e

Kwa maana ninapendezwa na mambo hayo,”^f asema Yehova.

25 “Tazama! Siku zinakuja,” asema Yehova, “nami nitamwadhibu* kila mtu aliye-tahiriwa lakini bado hajatahiriwa,^g **26** yaani, Misri^h na Yudaⁱ na Edomu^j na Waamoni^k na Moabu^l na wale wote wanaonyoa nywele pembeni mwa vichwa vyao ambao wanakaa nyikani;^m kwa maana mataifa yote hayajatahiriwa, na watu wote wa nyumba ya Israeli hawajatahiriwa moyoni.”ⁿ

10 Sikieni neno ambalo Yehova amesema dhidi yenu, enyi watu wa nyumba ya Israeli. **2** Yehova anasema hivi:

“Msijifunze njia ya mataifa,^o

Wala msihofu ishara za mbinguni

9:17 *Au “nyimbo za maombolezo.”
9:20 *Au “wimbo huu wa maombolezo.”

9:24 *Au “anayejisifu na ajisifu.” 9:25
*Au “nitamfanya awajibike.”

Kwa sababu mataifa yana-zihofu.^a

3 Kwa maana desturi za mataifa ni udanganyifu.*

Ni mti tu wa msituni ulio-katwa,

Uliochongwa kwa mikono ya fundi kwa kifaa chake.^{#b}

4 Wanaupamba kwa fedha na dhahabu^c

Wanaupigilia misumari kwa nyundo ili usianguke.^d

5 Kama sanamu ya kufukuza ndege katika shamba la matango, haziwezi kuzungumza;^e

Lazima zibebwe, kwa maana haziwezi kutembea.^f

Msiziogope kwa maana haziwezi kuwadhuru,

Wala haziwezi kufanya jambo lolote jema.^g

6 Hakuna yeyote aliyekama wewe, Ee Yehova.^h

Wewe ni mkuu, na jina lako ni kuu na lenye nguvu.

7 Ni nani asiyepaswa ku-kuogopa, Ee Mfalme wa mataifa,ⁱ kwa maana ni jambo linalofaa;

Kwa sababu kati ya watu wote wenye hekima wa mataifa na kati ya falme zao zote,

Hakuna yeyote yule aliyekama wewe.^j

8 Wote hawatamii akili nao ni wajinga.^k

Mafundisho kutoka kwa mti ni udanganyifu* mtupu.^l

9 Mabamba ya fedha hule-

10:3, 8 *Au "ubatili." 10:3 #Au "tezo yake."

SURA YA 10

a Isa 47:13

b Isa 40:20
Isa 44:14, 15
Isa 45:20
Hab 2:18

c Zb 115:4
Isa 40:19

d Isa 41:7

e Hab 2:19

f Isa 46:7

g Isa 41:23
Isa 44:9
IKo 8:4

h Kut 15:11
2Sa 7:22
Zb 86:8

i Zb 22:28

j Zb 89:6
Da 4:35

k Yer 51:17
Hab 2:18

l Isa 44:19

Safu ya 2

a 1Fa 10:22

b Yos 3:10
Da 6:26

c Da 4:3
Hab 1:12
Ufu 15:3

d Nah 1:5

e Isa 2:18
Yer 51:17, 18
Sef 2:11

f Met 3:19
Isa 45:18

g Zb 136:3, 5
Isa 40:22
Yer 51:15, 16

h Ayu 37:2
Ayu 38:34

i Ayu 36:27
Zb 135:7

j Mwa 8:1
Kut 14:21
Hes 11:31
Yon 1:4

twa kutoka Tarshishi^a na dhahabu kutoka Ufazi, Kazi ya fundi, ya mikono ya mhunzi.

Mavazi yao ni nyuzi za bluu na sufu ya zambarau.

Vyote hutengenezwa na wafanyakazi stadi.

10 Lakini kwa kweli Yehova ni Mungu.

Yeye ndiye Mungu aliyehai^b na Mfalme wa milele.^c

Kwa sababu ya ghadhabu yake dunia itatetemeka,^d Na hakuna taifa litakalostahimili shutuma yake.

11 * Waambieni hivi:

"Miungu ambayo haikuumba mbingu na dunia Itaangamia kutoka duniani na kutoka chini ya hizi mbingu."^e

12 Yeye ndiye Muumba wa dunia kwa nguvu zake, Yule aliyeiimarisha ardhi inayozaa kwa hekima yake^f

Na aliyemitandaza mbingu kwa uelewaji wake.^g

13 Anapofanya sauti yake isikike,

Maji yaliyo mbinguni husukasuka,^h

Naye huyafanya mawingu yapande* kutoka kwenye miisho ya dunia.ⁱ

Hutengeneza radi[#] kwa ajili ya mvua,

Naye huutoa upepo katika maghala yake.^j

14 Kila mtu anatenda bila kutumia akili na bila ujuzi.

10:11 *Mwanzoni, mstari wa 11 uliandiwa katika Kiaramu. **10:13** *Au "Huu-fanya mvuke upande." #Au labda, "malango."

Kila fundi wa chuma ataaibishwa kwa sababu ya sanamu ya kuchongwa,^a Kwa maana sanamu yake ya chuma* ni uwongo, Nazo hazina roho[#] ndani yake.^b

15 Sanamu hizo ni udanganifu,* kazi ya mzaha.^c Siku yao ya hukumu itakapofika, zitaangamia.

16 Fungu la Yakobo si kama vitu hivyo, Kwa maana Yeye ndiye aliyeumba kila kitu, Na Israeli ndiyo fimbo ya urithi wake.^d Yehova wa majeshi ndilo jina lake.^e

17 Kusanya mzigo wako kutoa ardhini, Ewe mwanamke uliyezinguirwa.

18 Kwa maana Yehova anasema hivi: "Tazama, ninawatupa* nje wakaaji wa dunia wakati huu,^f Nami nitawafanya wataabike."

19 Ole wangu kwa sababu ya jeraha langu!^{*g} Kidonda changu hakiwezi kupona. Nami nilisema: "Kwa hakika huu ni ugonjwa wangu, na lazima niuvumilie."

20 Hema langu limeharibiwa, na kamba zangu zote za mahema zimekatwa.^h Wanangu wameniacha na hawapo tena.ⁱ Hakuna yeyote aliyebaki

10:14 *Au "sanamu ya kuyeyushwa."
[#]Au "pumzi." 10:15 *Au "ubatili."
 10:18 *Au "ninawarusha." 10:19 *Au "jeraha langu la kuvunjika."

SURA YA 10

a Isa 42:17
Isa 44:11

b Yer 51:17
Hab 2:18, 19

c Isa 41:29

d Kum 32:9
Zb 135:4

e Isa 47:4

f Kum 28:63
Yer 16:13

g Yer 8:21

h Yer 4:20

i Yer 31:15

Safu ya 2

a Yer 5:31

b Yer 2:8
Yer 8:9

c Yer 23:1
Eze 34:5, 6

d Yer 1:15
Yer 4:6
Yer 6:22
Hab 1:6

e Yer 9:11

f Zb 17:5
Zb 37:23
Met 16:3
Met 20:24

g Zb 6:1
Zb 38:1

h Yer 30:11

i Isa 34:2

j Yer 51:34

k Isa 10:22

l Zb 79:6, 7
Yer 8:16
Omb 2:22

wa kulitandaza hema langu au kuviinua vitamba vyangu vya mahema.

21 Kwa maana wachungaji wametenda kwa upumbavu,^a

Wala hawajatafuta ushauri kutoka kwa Yehova.^b

Ndiyo sababu hawajatenda kwa ufahamu,

Na kondoo wao wote wametawanyika.^c

22 Sikiliza! Habari! Inakuja! Kishindo kikubwa kutoka nchi ya kaskazini,^d

Ili kuyafanya majiji ya Yuda yawe ukiwa, mapango ya mbwamwitu.^e

23 Ninajua vema, Ee Yehova, kwamba njia ya mwanaadamu haimo katika uwezo wake.

Mwanadamu anayetembea hana uwezo wa kuongoza hatua yake.^f

24 Nirekebishe, Ee Yehova, kulingana na hukumu, Lakini si katika hasira yako,^g usije ukanimaliza.^h

25 Yamwagie ghadhabu yako mataifa yanayokupuza!ⁱ Na familia ambazo hazililitii jina lako.

Kwa maana wamemnyafua Yakobo,^j

Naam, wamemnyafua na kumwangamiza kabisa,^k

Nao wameifanya nchi yake ukiwa.^l

11 Hili ndilo neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova, likisema: **2** "Enyi watu, sikieni maneno ya agano hili!

“Watangazie* maneno haya watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu, **3** nawe uwaa- mbie, ‘Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: “Amelaaniwa mtu asiyetii maneno ya agano hili,^a **4** niliyowaamuru mababu zenu siku niliyowatoa nchini Misri,^b kutoka katika tanuru la kuyeyushia chuma,^c nikisema, “Tiini sauti yangu, nanyi mfanye mambo yote ninayowaamuru; nanyi mtakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu,^d **5** ili nitimize kiapo nilichowaapia mababu zenu, kwamba nitawapa nchi inayotiririka maziwa na asali,^e kama ilivyo leo hii.””

Nami nikajibu: “Amina, * Ee Yehova.”

6 Kisha Yehova akaniambia: “Tangaza maneno haya yote katika majiji ya Yuda na kwnye barabara za Yerusalemu: ‘Sikieni maneno ya agano hili, na myatekeleze. **7** Kwa maana niliwaonya vikali mababu zenu siku niliyowatoa nchini Misri na mpaka leo hii, niliwaonya tena na tena: * “Tiini sauti yangu.”^f **8** Lakini hawakusikiliza wala kutega sikio lao; badala yake, kila mmoja wao aliendelea kuufuata kwa ukaidi moyo wake mwovu.^g Basi nikawaadhibu kulingana na maneno yote ya agano hili niliyowaamuru wafuate na ambayo walikataa kuyatekeleza.”

9 Kisha Yehova akaniambia: “Kuna njama kati ya watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu. **10** Wameyarudia makosa ya mababu zao wa zama-

11:2 *Inaonekana Yeremia ndiye anayeambiwa. **11:5** *Au “Na iwe hivyo!” **11:7** *Tnn., “nilikuwa nikiamka mapema na kuwaonya.”

SURA YA 11

a Kum 27:26
Kum 28:15

b Kut 24:3

c Kut 13:3
Kum 4:20

d Law 26:3, 12

e Mwa 15:18
Kut 3:8
Law 20:24
Kum 6:3

f Yer 7:13
Yer 25:4
Yer 35:15

g Isa 65:2
Yer 7:24, 26
Eze 20:8
Zek 7:11, 12

Safu ya 2

a Amu 2:11, 17
1Sa 8:8
2Fa 22:17

b 2Nya 28:22, 23

c Kum 31:16
2Fa 17:6, 7
Ho 6:7

d 2Fa 22:16
Yer 6:19
Eze 7:5

e Isa 1:15
Yer 14:12
Eze 8:16
Mik 3:4

f Kum 32:37, 38
Yer 2:28

g Yer 7:9, 10

h Yer 7:16
Yer 14:11

ni, waliokataa kutii maneno yangu.^a Wao pia wameifuata miungu mingine na kuiabu- du.^b Watu wa nyumba ya Israeli na wa nyumba ya Yuda wamevunja agano langu nililofanya pamoja na mababu zao.^c

11 Kwa hiyo Yehova anasema hivi: ‘Ninawaletea msiba^d ambao hawataweza kuupeuka. Watakaponiomba msaada, sitawasikiliza.^e **12** Kisha majiji ya Yuda na wakaaji wa Yerusalemu wataenda kwa miungu wanayoitolea dhabihu* na kuomba msaada,^f lakini kwa vyovyote vile haitawao- koa watakopopatwa na msiba. **13** Kwa maana miungu yenu imekuwa mingi kama majiji yenu, enyi watu wa Yuda, nanyi mmekitengenezea kitu cha aibu* madhabahu nyingi kama barabara zilizo Yerusalemu, madhabahu za kumtolea dhabihu Baali.’^g

14 “Lakini wewe,* usisali kwa ajili ya watu hawa. Usipaze kilio au kusali kwa ajili yao,^h kwa maana sitasikiliza watakaponililia kwa saba- bu ya msiba wao.

15 Mpendwa wangu ana haki gani ya kuwa katika nyumba yangu

Wakati watu wengi wame- tekeleza njama nyingi za uovu?

Je, kwa nyama takatifu* watauzuia msiba utaka- pokujia?

Je, utafurahi wakati huo?

16 Wakati fulani Yehova alikuwa mzeituni unaosi- tawi,

11:12 *Au “moshi wa dhabihu.” **11:13** *Au “mungu wa aibu.” **11:14** *Yaani, Yeremia. **11:15** *Yaani, dhabihu zilizo- tolewa hekaluni.

Maridadi na wenye matunda mazuri.

Kwa sauti yenye mngurumo mkubwa, ameuwasha moto mzeituni huo, Nao wamevunja matawi yake.

17 “Yehova wa majeshi, Aliyekupanda,^a ametangaza kwamba msiba utakujia wewe kwa sababu ya uovu uliote ndwa na watu wa nyumba ya Israeli na wa nyumba ya Yuda, ambao wamenikasirisha kwa kumtolea dhabihu Baali.”^b

18 Yehova alinijulisha ili ni jue;

Wakati huo ulinionesha mambo walivyokuwa wakitenda.

19 Nilikuwa kama mwana-kondoo mtulivu anayepelekwa machinjioni.

Sikujua kwamba walikuwa wakipanga njama dhidi yangu:^c

“Na tuuangamize ule mti na matunda yake,

Na tumkate kabisa kutoka kwenye nchi ya walio hai,

Ili jina lake lisikumbukwe kamwe.”

20 Lakini Yehova wa majeshi huhukumu kwa uadilifu; Huchunguza mawazo ya ndani kabisa* na pia moyo.^d

Acha nione ukiwalipiza kisasi,

Kwa maana nimeileta kesi yangu kwako.

21 Kwa hiyo Yehova anasema hivi dhidi ya watu wa Ana-

11:20 *Au “hisia za ndani kabisa.” Tnn., “figo.”

SURA YA 11

a Isa 5:2
Yer 2:21

b Yer 19:5, 15

c Yer 18:18

d 1Nya 28:9
Yer 17:10
Yer 20:12

Safu ya 2

a Yer 1:1

b Isa 30:10
Amo 2:12
Amo 7:16

c 2Nya 36:17
Omb 2:21

d Yer 18:21

e Yos 21:8, 18

SURA YA 12

f Mwa 18:25

g Ayu 12:6
Ayu 21:7
Zb 73:3
Yer 5:28

h Isa 29:13

i Zb 139:1, 2

j 2Fa 20:3
Zb 17:3
Yer 11:20

thothi^a wanaotaka kukuu* na wanaosema: “Usitabiri katika jina la Yehova,^b la sivyo tutakuu kwa mikono yetu”; **22** kwa hiyo Yehova wa majeshi anasema hivi: “Tazama, nitawaadhibu.* Vijana watakuu kwa upanga,^c na wanao wao na mabinti wao watakuu kwa njaa kali.^d **23** Hakuna yeyote atakayebaki kati yao, kwa maana nitawaletea msiba watu wa Anathothi^e katika mwaka wao wa kuadhibiwa.”*

12 Wewe ni mwadilifu, Ee Yehova,^f ninapokuletea malalamishi yangu,

Ninapozungumza nawe kuhusu mambo ya haki.

Lakini kwa nini njia ya waovu imefanikiwa,^g

Na kwa nini watu wenye hila hawana wasiwasi?

2 Uliwapanda, nao wametia mizizi.

Wamekua na kuzaa matunda.

Wewe uko kwenye midomo yao, lakini uko mbali na mawazo yao ya ndani kabisa.*^h

3 Lakini unanijua vema, Ee Yehova,ⁱ unaniona;

Umeuchunguza moyo wangu na kuupata ukiwa katika muungano nawe.^j

Waweke kando kama kondoo wa kuchinjwa,

Na uwatenge kwa ajili ya siku ya kuuawa.

4 Nchi itaendelea kunyauka mpaka lini

11:21 *Au “wanaoitafuta nafsi yako.”

11:22 *Au “nitawafanya wawajibike.”

11:23 *Au “kuwajibishwa.”

12:2 *Au “hisia zao za ndani kabisa.” Tnn., “figo zao.”

Na majani ya kila uwanja kukauka?^a

Kwa sababu ya uovu wa wale wanaokaa ndani yake,

Wanyama na ndege wamefagiliwa mbali.

Kwa maana wamesema: “Haoni kitakachotupata.”

- 5 Ikiwa unachoka unapokimbia pamoja na watu waendao kwa miguu, Unawezaje kushindana mbio na farasi?^b

Hata kama una uhakika katika nchi ya amani, Itakuwaje kwako kati ya vichaka vikubwa kando ya Yordani?

- 6 Kwa maana hata ndugu zako mwenyewe, nyumba ya baba yako mwenyewe, Wamekutendea kwa hila.^c Wamelia kwa sauti kubwa dhidi yako. Usiwe na imani nao, Hata wakikuambia mambo mema.

- 7 “Nimeiacha nyumba yangu;^d nimeuacha urithi wangu.^e

Mpendwa wangu nimpendaye sana* nimemtia mikononi mwa maadui wake.^f

- 8 Urithi wangu umekuwa kwangu kama simba msituni. Amenguruma dhidi yangu. Kwa hiyo nimemchukia.

- 9 Urithi wangu ni kama ndege anayewinda mwenye rangi nyingi;*

SURA YA 12

a Yer 14:6
Yer 23:10

b Yer 4:13

c Yer 9:4

d Lu 13:35

e Kut 19:5
Isa 47:6

f Omb 2:1

Safu ya 2

a 2Fa 24:2
Eze 16:37

b Isa 56:9
Yer 7:33

c Zb 80:8
Isa 5:1, 7
Yer 6:3

d Isa 63:18
Yer 3:19

e Yer 9:11
Yer 10:22

f Isa 42:24, 25

g Law 26:33
Yer 15:2

h Law 26:16
Mik 6:15

Ndege wengine wanaowinda wanamzunguka na kumshambulia.^a

Njoooni, kusanyikeni pamoja, ninyi nyote wanyama wa mwituni,

Njoooni mle.^b

- 10 Wachungaji wengine wameliharibu shamba langu la mizabibu;^c

Wamelikanyaga-kanyaga shamba langu.^d

Wameligeuza shamba langu linalotamanika kuwa nyika yenye ukiwa.

- 11 Limekuwa ukiwa; Limenyauka;* Limekuwa mahame mbele zangu.^e

Nchi yote imefanywa kuwa mahame,

Lakini hakuna mtu anayelitia jambo hilo moyoni.^f

- 12 Waangamizaji wamekuja kwenye vijija vyote vya nyikani vilivyokanyagwa sana,

Kwa maana upanga wa Yehova unanyafua kuanzia mwisho mmoja wa nchi mpaka mwisho wa pili.^g

Hakuna amani kwa yeyote.*

- 13 Wamepanda ngano, lakini wamevuna miiba.^h

Wamejichosha wenyewe, lakini hawajapata faida yoyote.

Wataona aibu kwa sababu ya mazao yao

Kwa sababu ya hasira ya Yehova inayowaka.”

- 14 Yehova anasema hivi dhidi ya majirani wangu wote waovu, wanaogusa urithi ni-

12:7 *Au “Mpendwa wa nafsi yangu.”

12:9 *Au “mwenye madoadao.”

12:11 *Au labda, “Linaomboleza.”

12:12 *Tnn., “wote wenye mwili.”

liowamilikisha watu wangu Waisraeli:^a “Tazama, nina-wang’oa kutoka kwenye nchi yao,^b nami nitawang’oa watu wa nyumba ya Yuda kuto-ka kati yao. **15** Lakini baada ya kuwang’oa, nitawaonyesha tena rehema na kumrudisha kila mmoja wao kwenye urithi wake na kwenye ardhi yake.”

16 “Na wakihakikisha kwa-amba wanajifunza njia za watu wangu na kuapa kwa jina lan-gu, ‘Kwa hakika kama Yehova anavyoishi!’ kama walivyo-wafundisha watu wangu kua-pa kwa jina la Baali, ndipo wa-takapojengwa miongoni mwa watu wangu. **17** Lakini wa-kiyataa kutii, mimi pia nitaling’oa taifa hilo, nitaling’oa na kuliangamiza,” asema Yehova.^c

13 Yehova aliniambia hivi: “Nenda ukajinunulie mshipi wa kitani ujifunge kiunoni, lakini usiutie ndani ya maji.” **2** Basi nikanunua mshipi kulingana na neno la Yehova nikajifunga kiunoni. **3** Na neno la Yehova likanijia mara ya pili likisema: **4** “Uchukue mshipi ulionunua ambao umejifunga, nawe uinuke na kwenda kwenye Mto Efrati, uufiche huko katika mpasuko wa jabali.” **5** Basi nikaenda, nikauficha kando ya Mto Efrati, kama Yehova alivyoniama.

6 Lakini baada ya siku nyin-gi Yehova akaniambia: “Inu-ka, nenda kwenye Mto Efra-ti, uchukue kutoka huko ule mshipi niliokuamuru uufiche huko.” **7** Basi nikaenda kwe-nye Mto Efrati, nikachimba na kuuchukua ule mshipi kutoka mahali nilipouficha, nami ni-

SURA YA 12

a Zb 79:4
Yer 48:26
Eze 25:3
Zek 1:15
Zek 2:8

b Yer 48:2
Yer 49:2

c Isa 60:12

Safu ya 2

SURA YA 13

a Law 26:19
Sef 3:11

b 2Nya 36:15, 16

c Yer 6:28

d Kut 19:5
Kum 26:18
Zb 135:4

e Yer 33:9

f Yer 6:17

g Isa 29:9
Isa 51:17
Yer 25:27

h Yer 6:21
Eze 5:10

i Eze 7:4
Eze 24:14

kaona kwamba mshipi huo uli-kuwa umeharibika; haukufaa kabisa.

8 Kisha neno la Yehova likanijia likisema: **9** “Yehova anasema hivi, ‘Hivyo ndivyo nitakavyokiharibu kiburi cha Yuda na kiburi kingi cha Yeru-salemu.’ **10** Watu hawa wao-vu wanaokataa kutii maneno yangu,^b wanaofuata kwa ukai-di moyo wao wenyewe,^c na wa-naofuata miungu mingine, wa-kiiabudu na kuiinamia, wata-kuwa kama mshipi huu usio-faa kabisa.’ **11** ‘Kwa maana kama vile mshipi unavyoshi-kamana na kiuno cha mtu, ndivyo nilivyowafanya watu wote wa nyumba ya Israeli na watu wote wa nyumba ya Yuda washikamane nami,’ asema Yehova, ‘ili wawe watu wan-gu,^d jina,^e sifa, na kitu ma-ridadi kwangu. Lakini hawa-kutii.’^f

12 “Nawe unapaswa pia ku-wapa ujumbe huu: ‘Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: “Kila mtungi mkubwa unapaswa kujazwa divai.” Nao watakujibu, ‘Je, tayari hatujui kwamba kila mtungi mkubwa unapaswa kujazwa divai?’ **13** Kisha uwaambie, ‘Yehova anasema hivi: “Taza-ma, ninawajaza ulevi wakaa-ji wote wa nchi hii,^g wafal-me wanaoketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi, makuhani na manabii, na wakaaji wote wa Yerusalemu. **14** Nami ni-tawaponda kwa kuwagongani-sha mtu na mwenzake, baba na wana pia,” asema Yehova.^h “Sitawahurumia wala kuwasi-kitikia kamwe wala kuwaonye-sha rehema yoyote; hakuna kitakachonizua nisiwaanga-mize.”ⁱ

- 15** Sikieni na mtege sikio.
Msiwe na kiburi, kwa maana Yehova amesema.
- 16** Mtukuzeni Yehova Mungu wenu
Kabla hajaleta giza
Na kabla miguu yenu haijajikwaa kwenye milima jioni.
Mtatumaini kupata nuru,
Lakini ataleta kivuli kizito;
Ataigeuza nuru iwe giza zito.^a
- 17** Nanyi mkikataa kusikiliza,
Nitalia* kisiri kwa sababu ya kiburi chenu.
Nitatoa machozi mengi, na macho yangu yatabubuji-
ka machozi,^b
Kwa sababu kondoo wa Yehova^c wamechukuliwa mateka.
- 18** Mwambie mfalme na mama malkia,^d ‘Ketini mahali pa chini,
Kwa maana taji lenu maridadi litaanguka kutoka kwenye vichwa vyenu.’
- 19** Majiji ya kusini yamefungwa,* na hakuna mtu wa kuyafungua.
Watu wote wa Yuda wamepeleka uhamishoni, wamepeleka kabisa uhamishoni.^e
- 20** Inua macho yako uwaone wale wanaokuja kutoka kaskazini.^f
Liko wapi kundi ulilopewa, kondoo wako maridadi?^g
- 21** Itasema nini adhabu yako utakapofika
Kutoka kwa marafiki wako wa karibu uliowafundi-
sha tangu mwanzo?^h

13:17 *Au “Nafsi yangu italia.” 13:19 *Au “yamezingirwa.”

SURA YA 13

a Isa 59:9

b Yer 9:1

c Zb 100:3

d 2Fa 24:12
Yer 22:24, 26

e Kum 28:64

f Yer 6:22

g Eze 34:8

h Isa 39:1, 2

Safu ya 2

a Yer 6:24
Mik 4:9b Yer 5:19
Yer 16:10, 11

c Eze 16:37

d Met 27:22

e Law 26:33
Kum 28:64

f Yer 2:32

g Kum 32:37, 38
Isa 28:15
Yer 10:14h Omb 1:8
Eze 16:37
Eze 23:29i Yer 2:20
Eze 16:15j Isa 65:7
Eze 6:13

k Eze 24:13

SURA YA 14

l Kum 28:24

- Je, hutashikwa na uchungu wa kuzaa, kama wa mwanamke anayezaa?^a
- 22** Nawe ukijiuliza moyoni mwako, ‘Kwa nini nimepatwa na mambo haya?’^b
Umevuliwa nguo yako kwa sababu ya kosa lako kubwa^c
Na visigino vyako vimetendewa kikatili.
- 23** Je, Mkushi* anaweza kuitadili ngozi yake, au chui madoa yake?^d
Kama inawezekana, basi mnaweza kutenda mema,
Ninyi mliozoezwa kutenda uovu.
- 24** Basi nitawatawanya kama nyasi kavu zinazopeperushwa na upepo wa jangwani.^e
- 25** Hii ndiyo kura yako, fungu nililokupimia,” asema Yehova,
“Kwa sababu umenisahau^f nawe unautumaini uwongo.^g
- 26** Kwa hiyo, nitainua nguo yako juu ya uso wako,
Na aibu yako itaonekana,^h
- 27** Matendo yako ya uzinziⁱ na kilio chako cha uchu, Ukahaba wako uliopotoka.*
Juu ya vilima, katika mashamba,
Nimeyaona matendo yako yanayochukiza.^j
Ole wako, Ee Yerusalemu!
Utaendelea kuya mchafu mpaka lini?”^k
- 14** Hili ndilo neno la Yehova lililomjia Yereima kuhusu ukame:^l

13:23 *Au “Mwethiopia.” 13:27 *Au “wa aibu.”

- 2** Yuda inaomboleza,^a na malango yake yamefifia. Yamehuzunika na kuzama ardhini, Na kilio kinapanda juu kutoka Yerusalemu.
- 3** Na mabwana wao wanawatuma watumishi wao* walete maji. Wanaenda kwenye visima[#] lakini hawapati maji. Wanarudi vyombo vyao vikiwa vitupu. Wameaibika na kukata tamaa, Nao wanavifunika vichwa vyao.
- 4** Kwa sababu udongo umeapasuka, Kwa maana hakuna mvua nchini,^b Wakulima wametamauka na kuvifunika vichwa vyao.
- 5** Hata paa jike aliye porini anamwacha mtoto wake mchanga Kwa sababu hakuna nyasi.
- 6** Punda wa mwituni wanasi-mama kwenye vilima vitupu. Wanahemahema kama mbwamwitu; Macho yao yanadhoofika kwa sababu hakuna majani.^c
- 7** Ingawa makosa yetu yantushtaki, Ee Yehova, tenda kwa ajili ya jina lako.^d Kwa maana matendo yetu ya ukosefu wa uaminifu ni mengi,^e Nasi tumekutendea dhambi.

14:3 *Au "walio wadogo nchini." [#]Au "mitaro; matangi."

SURA YA 14

a Yoe 1:10

b Law 26:20
Kum 28:23c Yer 12:4
Yoe 1:18d Yos 7:9
Zb 25:11
Zb 115:1, 2e Ezz 9:6
Ne 9:33
Da 9:5, 8

Safu ya 2

a Zb 106:8
Zb 106:21
Isa 45:15b Kut 29:45
Kum 23:14

c Da 9:19

d Yer 2:23

e Yer 2:25

f Yer 6:20

g Ho 8:13

h Yer 7:16
Yer 11:14i Isa 1:15
Isa 58:3
Yer 11:11
Eze 8:18

j Isa 1:11

k Yer 9:16
Eze 5:12l Yer 4:10
Yer 5:31
Yer 6:13, 14
Yer 23:16, 17
Yer 27:8-10
Eze 13:10
Mik 3:11m Yer 23:25, 26
Yer 29:21

- 8** Ee tumaini la Israeli, Mwo-kozi wake^a wakati wa taabu, Kwa nini wewe ni kama mgeni nchini, Kama msafiri alalaye usiku mmoja tu?
- 9** Kwa nini wewe ni kama mtu anayeshangaa, Kama mwanamume mwenye nguvu asiyeweza kuokoa? Kwa maana uko miongoni mwetu, Ee Yehova,^b Nasi tumeitwa kwa jina lako.^c Usituache.

10 Yehova anasema hivi kuhusu watu hawa: "Wanapenda kutangatanga;^d hawajaizuia miguu yao.^e Basi Yehova hafurahishwi nao.^f Sasa ataliku- mbuka kosa lao, naye atawaa- dhibu^g kwa sababu ya dhambi zao."^g

11 Kisha Yehova akania- mbia: "Usisali kwamba watu hawa wapate mema.^h **12** Wanapofunga, sisikilizi sihi zao,ⁱ na wanapotoa dhabihu nzima za kuteketezwa na matoleo ya nafaka, siyafurahii,^j kwa maana nitawaangamiza kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari."^k

13 Ndipo nikasema: "Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Tazama, manabii wanawaambia, 'Hamtaona upanga, wala hamta- kumbwa na njaa kali, bali nitawapa amani ya kweli mahali hapa.'^l"

14 Kisha Yehova akania- mbia: "Manabii wanatabiri uwongo katika jina langu.^m Si- kuwatuma wala kuwaamuru

14:10 *Au "atawafanya wawajibike."

wala kuzungumza nao.^a Wanawatabiria ninyi maono ya uwongo na uaguzi* usiofaa kitu na udanganyifu wa moyo wao wenyewe.^b **15** Kwa hiyo mimi Yehova ninasema hivi kuhusu manabii wanaotabiri katika jina langu ingawa sikuwatuma, na wanaosema hakuna upanga wala njaa kali itakayokuja katika nchi hii: ‘Manabii hao wataangamia kwa upanga na kwa njaa kali.’^c **16** Na watu wanaotabiriwa mambo hayo watatupwa katika barabara za Yerusalemu kwa sababu ya njaa kali na upanga, na hakuna yeyote atakayewazika^d—wao, wake zao, wana wao, au mabinti wao—kwa maana nitawamwagia msiba wanaostahili.’^e

17 “Unapaswa kuwaambia neno hili,

‘Macho yangu na yabubu-jike machozi usiku na mchana, yasiishe,^f

Kwa maana bikira, binti ya watu wangu amepondwa kabisa na kuvunjwa,^g

Kwa jeraha baya sana.

18 Nikienda shambani na kutazama,

Ninawaona wale waliouawa kwa upanga!^h

Na nikiingia jijini,

Ninayaona magonjwa yaliyoletwa na njaa kali!ⁱ

Kwa maana nabii na kuhani wamezunguka katika nchi wasiyoiuja.”^j

19 Je, umeikataa Yuda kabisa, au, je, umelichukia* Sayuni kabisa?^k

Kwa nini umetupiga, hivi kwamba hatuwezi ku-pona?^l

SURA YA 14

a Yer 23:21
Yer 27:15

b Omb 2:14

c Yer 5:12, 13
Yer 23:15
Eze 12:24
Eze 13:9

d Zb 79:2, 3
Yer 9:22

e Yer 4:18

f Yer 8:18, 21
Yer 9:1

g Omb 1:15

h Eze 7:15

i Omb 5:10

j Kum 28:36

k Yer 12:8
Omb 5:22

l 2Nya 36:15, 16

Safu ya 2

a Yer 8:15

b Ezr 9:7
Da 9:5, 8

c Eze 36:22
Da 9:15

d Kut 32:13
Law 26:41, 42
Zb 106:43-45

e Kum 28:12
Isa 30:23
Yoe 2:23

SURA YA 15

f Kut 32:11
1Sa 7:9
Zb 99:6
Zb 106:23

g Eze 5:2

Tulitumaini kupata amani, lakini hakuna jambo lolote jema lililokuja, Wakati wa kuponywa, lakini kuna hofu!^a

20 Tunatambua uovu wetu, Ee Yehova,

Na kosa la mababu zetu, Kwa maana tumekutendea dhambi.^b

21 Kwa ajili ya jina lako, usitukatae;^c

Usikidharau kiti chako cha ufalme chenye utukufu.

Kumbuka, nawe usivunje agano lako pamoja nasi.^d

22 Je, kuna sanamu yoyote kati ya sanamu za ubatili za mataifa inayoweza kuleta mvua,

Au, je, hata mbingu zinaweza kuleta mvua zenyewe?

Je, si Wewe peke yako, Ee Yehova Mungu wetu?^e

Nasi tunakutumaini, Kwa maana wewe peke yako ndiye uliyefanya mambo hayo yote.

15 Kisha Yehova akaniaambia: “Hata kama Musa na Samweli wangekuwa wamesimama mbele zangu,^f singewaonyesha kibali* watu hawa. Wafukuze kutoka mbele zangu. Waache waende.

2 Nao wakikuuliza, ‘Twende wapi?’ unapaswa kuwaambia, ‘Yehova anasema hivi:

“Yeyote aliyekusudiwa kufa kwa ugonjwa unaoua, na afe kwa ugonjwa unaoua!

Yeyote aliyekusudiwa kufa kwa upanga, na afe kwa upanga!^g

14:14 *Au “ubashiri.” 14:19 *Au “nafsi yako imelichukia.”

15:1 *Au “nafsi yangu haingewaelekea.”

Yeyote aliyekusudiwa kufa kwa njaa kali, na afe kwa njaa kali!

Na yeyote aliyekusudiwa kwenda utekwani, na aende utekwani!"^a

3 "Nami nitawaletea misiba minne,^{*b} asema Yehova, 'upanga ili kuua, mbwa ili kukokota, na ndege wa angani na wanyama wa duniani ili kula na kuharibu.^c **4** Nami nitawafanya wawe kitu cha kutisha kwa falme zote za dunia^d kwa sababu ya Manase mwana wa Hezekia, mfalme wa Yuda, kwa sababu ya mambo aliyofanya Yerusalemu.^e

5 Ni nani atakayekuhurumia, Ee Yerusalemu, Ni nani atakayekusikitikia, Na ni nani atakayesimama ili kuuliza kuhusu hali yako?"

6 'Umeniacha mimi,' asema Yehova.^f
'Unaendelea kunigeuzia mgongo.^{*g}

Basi nitaunyoosha mkono wangu dhidi yako na ku-kuangamiza.^h

Nimechoka kukuhurumia.[#]

7 Nami nitawapepeta kwa uma kwenye malango ya nchi.

Nitawaua watoto wao.ⁱ

Nitawaangamiza watu wangu,

Kwa sababu wanakataa kuziacha njia zao.^j

8 Wajane wao watakuwa

SURA YA 15

a Eze 12:11

b Eze 14:21

c Kum 28:26
Yer 7:33

d Kum 28:15, 25
Yer 24:9
Eze 23:46

e 2Fa 21:11
2Fa 23:26
2Fa 24:3, 4

f Yer 2:13

g Isa 1:4

h Sef 1:4

i Kum 28:15, 18
Yer 9:21
Eze 24:21

j Yer 5:3

Safu ya 2

a Yer 44:27
Eze 5:12

b Yer 20:14

c Yer 20:5

wengi mbele zangu kuli-ko mchanga wa bahari.

Nitaleta mwangamizaji dhidi yao wakati wa aduhuri, dhidi ya akina mama na vijana.

Nitawaletea wasiwasi na hofu kwa ghafla.

9 Mwanamke aliyezaa wato-to saba amedhoofika; Anapumua^{*} kwa shida. Jua lake limetua wakati bado ni mchana, Na kusababisha aibu na fedheha."[#]

'Na wachache waliobaki kati yao

Nitawaacha waangamizwe kwa upanga na maadui wao,' asema Yehova."^a

10 Ole wangu, ewe mama yangu, kwa sababu uliniza,^b

Mtu anayegombana na kuzozana daima na nchi yote.

Sijamkopesha mtu wala kukopesha;

Lakini wote wananilaani.

11 Yehova alisema: "Kwa hakika nitakuhudumia ili upate mema;

Kwa hakika nitakusaidia wakati wa msiba,

Wakati wa taabu dhidi ya adui.

12 Je, kuna yeyote anaye-weza kuvunja chuma vipandevipande, Chuma kutoka kaskazini, na shaba?

13 Nitatoa mali zako na hazina zako ili ziporwe,^c Bila malipo, kwa sababu

15:3 *Au labda, "aina nne za hukumu." Tnn., "familia nne." 15:6 *Au labda, "Unatembea ukirudi nyuma." #Au "kughairi."

15:9 *Au "Nafsi yake inapumua." #Au labda, "Limeaibishwa na kufedhehesha."

ya dhambi zako zote katika maeneo yako yote.

- 14** Nitawapatia maadui wenu Wazipeleke katika nchi msiyoiujua.^a

Kwa maana moto umewashwa kwa hasira yangu. Nao unawaka dhidi yenu.”^b

- 15** Wewe unajua, Ee Yehova, Nikumbuke na unikazie fikira.

Nilipizie kisasi wanaonitesta.^c

Usiache niangamie* kwa sababu wewe hukasiriki upesi.

Ujue kwamba ninabeba shutuma hii kwa sababu yako.^d

- 16** Maneno yako yalipatika-na, nami nikayala;^e Na neno lako likawa furaha na shangwe ya moyo wangu,

Kwa maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Yehova Mungu wa majeshi.

- 17** Siketi pamoja na watu wanaopenda raha na ku-shangilia.^f

Kwa sababu mkono wako uko juu yangu, ninaketi peke yangu,

Kwa maana umenijaza ghadhabu.^{*g}

- 18** Kwa nini maumivu yangu ni ya kudumu na jeraha langu haliponi?

Linakataa kupona.

Je, utakuwa kwangu kama chanzo cha maji cha udanganyifu,

Ambacho hakiwezi kute-gemeka?

- 19** Kwa hiyo Yehova anasema hivi:

15:15 *Tnn., “Usiniondolee mbali.”

15:17 *Au “ujumbe wa shutuma.”

SURA YA 15

a Law 26:38
Yer 16:13

b Kum 32:22
Isa 42:24, 25
Yer 17:4

c Yer 11:20
Yer 12:3
Yer 17:18
Yer 37:15

d Zb 69:7

e Eze 3:1-3
Ufu 10:9, 10

f Zb 1:1

g Yer 20:8

Safu ya 2

a Yer 1:18
Eze 3:9

b Yer 20:11

SURA YA 16

c Yer 15:2

d Zb 79:2, 3
Isa 5:25
Yer 7:33
Yer 9:22
Yer 36:30

e Eze 5:12

“Ukirudi, basi nitakurudisha,

Nawe utasimama mbele zangu.

Kiwa utatenganisha kili-cho na thamani kutoka kwa kisicho na thamani, Utakuwa kama kinywa changu mwenyewe.*

Watalazimika kuja kwako, Lakini wewe hutaenda kwao.”

- 20** “Ninakufanya kuwa ukuta wa shaba wenye ngome kwa watu hawa.^a

Kwa hakika watapigana nawe,

Lakini hawatakushinda,^b

Kwa maana mimi niko pamoja nawe, ili nikuokoe na kukukomboa,” asema Yehova.

- 21** “Nami nitakuokoa kutoka mikononi mwa watu waovu

Na kukukomboa kutoka mikononi mwa watu wakatili.”

16 Na neno la Yehova likanijia tena, likisema:

2 “Usioe mke, wala usiwe na wana na mabinti mahali hapa.

3 Kwa maana Yehova anasema hivi kuhusu wana na mabinti wanaozaliwa hapa na kuhusu mama zao wanaowazaa na kuhusu baba zao wanaowazaa katika nchi hii: **4** ‘Watakufa kwa magonjwa hatari,^c lakini hakuna atakaye-waombolezea wala kuwazika; watakuwa kama mbolea kwenye ardhi.^d Wataangamia kwa upanga na kwa njaa kali,^e na maiti zao zitakuwa chakula cha ndege wa angani na wanyama wa duniani.’

15:19 *Au “utakuwa msemaji wangu.”

5 “Kwa maana Yehova anasema hivi:

‘Usiingie katika nyumba ambamo waombolezaji wanafanya karamu, Wala usiende kuomboleza au kuwapa pole,’^a

‘Kwa maana nimewaondolea watu hawa amani yangu,’ asema Yehova,

‘Pamoja na upendo wangu mshikamanifu na rehema.’^b

6 Wakubwa kwa wadogo watakuwa katika nchi hii.

Hawatazikwa, Hakuna mtu atakayewao- mbolezea,

Wala hakuna mtu atakayejikatakata wala kujitia upara kwa ajili yao.*

7 Na hakuna mtu atakayewapa chakula wale wanaoomboleza,

Ili kuwafaraji baada ya kufiwa;

Wala hakuna yeyote atakayewapa kikombe cha faraja

Ili wanywe kwa sababu ya kumpoteza baba yao au mama yao.

8 Nawe usiingie katika nyumba ya karamu

Kuketi pamoja nao ili kula na kunywa.’

9 “Kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Mahali hapa, katika siku zenu na mbele ya macho yenu wenyewe, nitazikomeshia sauti za furaha na shangwe, sauti ya bwana harusi na sauti ya bibi harusi.’^c

16:6 *Desturi za kipagani za kuomboleza ambazo inaelekea zilifanywa katika nchi ya Israeli iliyoasi imani.

SURA YA 16

a Eze 24:16, 17

b Kum 31:17
Isa 27:11
Isa 63:10

c Isa 24:7, 8
Yer 7:34
Ufu 18:23

Safu ya 2

a Yer 5:19

b Amu 2:12

c Yer 8:1, 2

d Da 9:11
Amo 2:4

e Yer 7:26

f Ne 9:29
Yer 6:28

g 2Nya 7:20
Yer 15:14
Yer 17:4

h Kum 4:27, 28
Kum 28:36

i Kut 20:2
Yer 23:7, 8

j Kum 30:1-3
Yer 3:18
Yer 24:6
Yer 30:3
Yer 32:37
Amo 9:14

10 “Utakapowaambia watu hawa maneno haya yote, watakuuliza, ‘Kwa nini Yehova amesema kwamba tutapatwa na msiba wote huu mkubwa? Tumemtendea Yehova Mungu wetu kosa gani na dhambi gani?’^a 11 Utawajibu, “Kwa sababu mababu zenu waliniacha,”^b asema Yehova, “nao waliendelea kuifuata miungu mingine na kuiabudu na kuiinama.^c Lakini waliniacha mimi, nao hawakuishika sheria yangu.”^d 12 Nanyi mmetenda mambo mabaya zaidi kuliko mababu zenu,^e na kila mmoja wenu anaufuata ukaidi wa moyo wake mwovu badala ya kunitii.^f 13 Basi nitawatupa nje ya nchi hii mpaka kwenye nchi ambayo wala ninyi wala mababu zenu hawakuujua,^g na huko mtalazimika kuiabudu miungu mingine mchana na usiku,^h kwa sababu sitawoonyesha kibali.”

14 “‘Hata hivyo, siku zinakuja,’ asema Yehova, ‘wakati ambapo hawatasema tena: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, aliyewatoa watu wa Israeli nchini Misri!”ⁱ 15 badala yake watasema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, aliyewatoa watu wa Israeli katika nchi ya kaskazini na katika nchi zote ambako alikuwa amewatawanya!” nami nitawarudisha katika nchi yao, niliyowapa mababu zao.’^j

16 “Tazama, ninawaita wavuvi wengi,’ asema Yehova, ‘Nao watawawua.

Na baada ya hapo nitawaita wawindaji wengi,

Nao watawawinda kwenye kila mlima na kila kilima

Na kutoka kwenye mipasuko ya majabali.

- 17 Kwa maana macho yangu yanaona kila kitu wanachofanya.*

Hawajafichwa kutoka mbele zangu,

Wala kosa lao halijafichwa kutoka mbele ya macho yangu.

- 18 Kwanza, nitalipa kiwango kamili kinachostahili kosa lao na dhambi yao,^a

Kwa maana wameitia unajisi nchi yangu kwa mifano isiyo hai ya* sanamu zao zinazochukiza

Nao wameujaza urithi wangu mambo yao yanayochukiza.”^b

- 19 Ee Yehova, nguvu zangu na ngome yangu, Kimbilio langu katika siku ya taabu,^c

Mataifa yatakuja kwako kutoka kwenye miisho ya dunia,

Nayo yatasema: “Mababu zetu walirithi uwongo mtupu,

Ubatili na vitu visivyofaa kitu ambavyo havina faida yoyote.”^d

- 20 Je, mwanadamu anaweza kujitengenezea miungu Wakati kwa kweli hiyo si miungu?^e

- 21 “Basi nitawafanya wajue, Wakati huu nitawafanya wajue nguvu zangu na uwezo wangu, Nao watalazimika kujua kwamba jina langu ni Yehova.”

16:17 *Au “yanatazama njia zao zote.”

16:18 *Tnn., “maiti za.”

SURA YA 16

a Isa 40:2

b Law 26:30
Zb 106:38

c Yer 17:17

d Yer 10:5, 14

e Zb 115:4
Yer 2:11
1Ko 8:4

Safu ya 2

SURA YA 17

a Amu 3:7
2Nya 24:18
2Nya 33:1, 3

b Isa 1:29
Eze 6:13

c 2Fa 24:11, 13
Yer 15:13

d Law 26:30
Eze 6:3

e Omb 5:2

f Kum 28:48
Yer 16:13

g Isa 5:25
Yer 15:14

h Isa 30:1, 2

i 2Fa 16:7

- 17 “Dhambi ya Yuda imeandikwa kwa kalamu ya chuma.

Imechongwa kwa ncha ya almasi juu ya bamba la moyo wao

Na juu ya pembe za madhabahu zao,

- 2 Huku wana wao wakiumbuka madhabahu zao na miti yao mitakatifu*^a Kando ya mti wenye majani mengi, juu ya vilima virefu,^b

- 3 Juu ya milima katika maeneo yaliyo wazi ya mashambani.

Mali zako, hazina zako zote, nitazitoa ili ziporwe^c

—Naam, mahali pako pa juu kwa sababu ya dhambi katika maeneo yako yote.^d

- 4 Utauacha kwa kupenda urithi wako niliokupa.^e

Nami nitakufanya uwa-tumikie maadui wako katika nchi usiyojua,^f

Kwa maana umeiwasha hasira yangu kama moto.*^g Itaendelea kuwaka daima.”

- 5 Yehova anasema hivi: “Amelaaniwa mtu* anayewatumaini wanadamu,^h Anayetegemea nguvu za wanadamu,^{#i}

Na ambaye moyo wake unamwacha Yehova.

- 6 Atakuwa kama mti ulio peke yake jangwani. Hataona mema yatakopkuja,

17:2 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 17:4 *Au labda, “Kwa hasira yangu umewashwa kama moto.” 17:5 *Au “mtu mwenye nguvu.” #Tnn., “Anayefanya mwili wa nyama kuwa mkono wake.”

Lakini atakaa mahali pakavu nyikani,
Katika nchi yenye chumvi ambayo hakuna mtu anayeweza kuishi ndani yake.

- 7** Amebarikiwa mtu* anayemtumaini Yehova, Ambaye uhakika wake uko katika Yehova.^a
- 8** Atakuwa kama mti uliopa-ndwa kando ya maji, Unaopeleka mizizi yake kwenye kijito. Hatatambua joto linapokuja, Bali majani yake yatasitawi sikuzote.^b Naye hatakuwa na mahangaiko katika mwaka wa ukame, Wala hataacha kuzaa matunda.
- 9** Moyo ni wenye hila* kuliko kitu kingine chochote nao ni hatari.^{#c} Ni nani anayeweza kuujua?
- 10** Mimi, Yehova, ninauchunguza moyo,^d Ninakagua mawazo ya ndani kabisa,* Ili kumpa kila mmoja kulingana na njia zake, Kulingana na matunda ya matendo yake.^e
- 11** Kama kwale anayekusanya kile ambacho hakutaga, Ndivyo alivyo mtu anayekusanya utajiri kwa udanganyifu.*^f Atauacha katikati ya masha yake,

17:7 *Au "mtu mwenye nguvu." 17:9 *Au "ni mdanganyifu." #Au labda, "hauwezi kuponywa." 17:10 *Au "hisia za ndani kabisa." Tnn., "figo." 17:11 *Au "lakini si kwa haki."

SURA YA 17

a Zb 34:8
Zb 146:5
Isa 26:3

b Zb 1:3
Zb 92:12, 13

c Mwa 6:5
Mwa 8:21
Met 28:26

d 1Sa 16:7
1Nya 28:9
Met 17:3
Met 21:2

e Ro 2:6
Gal 6:7
Ufu 2:23
Ufu 22:12

f Met 28:20
Isa 1:23
Yak 5:4

Safu ya 2

a 2Nya 2:5
Isa 6:1

b Zb 73:27
Isa 1:28

c Yer 2:13
Ufu 22:1

d Yer 15:20

e Isa 5:19
2Pe 3:4

f Yer 15:15
Yer 20:11

Na mwishowe ataonekana hana akili."

- 12** Kiti cha ufalme chenye utukufu, kilichokwezwa tangu mwanzo, Ndicho mahali petu patakatifu.^a
- 13** Ee Yehova, tumaini la Israeli, Wote wanaokuacha wataaibishwa. Wale wanaokuasi* wataandikwa mavumbini,^b Kwa sababu wamemwacha Yehova, chanzo cha maji yaliyo hai.^c
- 14** Niponye, Ee Yehova, nami nitapona. Niokoe, nami nitaokoka,^d Kwa maana ninakusifu wewe.
- 15** Tazama! Kuna wale wanaoniambia: "Neno la Yehova liko wapi?"^e Na lije, tafadhali!"
- 16** Lakini mimi, sikukimbia na kuacha kukufuata ukiwa mchungaji, Wala sikutamani siku ya msiba. Unajua vema mambo yote ambayo midomo yangu imesema; Yote yalitendeka mbele za uso wako!
- 17** Usiwe tisho kwangu. Wewe ni kimbilio langu katika siku ya msiba.
- 18** Wale wanaonitesa na waaibishwe,^f Lakini usiruhusu niaibishwe. Waache washikwe na hofu, Lakini usiruhusu nishikwe na hofu.

17:13 *Tnn., "wanaoniasi," inaelekea wanamwasi Yehova.

Ilete siku ya msiba juu yao,^a

Nawe uwaponde na kuwaagamiza kabisa.*

19 Yehova aliniambia hivi: “Nenda usimame katika lango la wana wa watu ambalo wafalme wa Yuda huingilia na kutokea, na katika malango yote ya Yerusalemu.^b

20 Nawe unapaswa kuwaambia hivi: ‘Sikieni neno la Yehova, ninyi wafalme wa Yuda, watu wote wa Yuda, na wakaaji wote wa Yerusalemu, mnaoingia kupitia malango haya.

21 Yehova anasema hivi: “Jihadharini, nanyi msibebe mzigo wowote siku ya Sabato wala kuingiza kupitia malango ya Yerusalemu.^c **22** Hampaswi kutoa mzigo wowote katika nyumba zenu siku ya Sabato; nanyi hampaswi kufanya kazi yoyote.^d Endeeleni kuishika siku ya Sabato ikiwa siku takatifu, kama nilivyowaamuru mababu zenu.^e **23** Lakini hawakusikiliza wala kutega sikio lao, nao wakakataa kwa ukaidi* kutii au kukubali nidhamu.”^f

24 ““Hata hivyo, mkinitii kabisa,” asema Yehova, “nanyi msiingize mzigo wowote kupitia malango ya jiji hili siku ya Sabato, nanyi mwendeele kuishika siku ya Sabato ikiwa siku takatifu kwa kutofanya kazi yoyote siku hiyo,^g **25** ndipo wafalme na wakuu wanaoketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi^h wataingia pia kupitia malango ya jiji hili, wakipanda gari na farasi, wao pamoja na wakuu wao, watu wa Yuda na wakaaji wa

17:18 *Au “uwaagamize mara mbili zaidi.” 17:23 *Tnn., “wakazifanya shingo zao kuwa ngumu.”

SURA YA 17

a Yer 18:23

b Yer 7:2

c Ne 13:19

d Kut 20:9, 10
Law 23:3

e Kut 31:13

f Isa 48:4
Eze 20:13

g Kum 5:12-14

h Zb 132:11

Safu ya 2

a Yer 22:4

b Yer 32:44

c Yer 33:13

d Law 1:3

e Ezr 3:3

f Law 2:1, 2

g Zb 107:22
Zb 116:17
Yer 33:10, 11h 2Fa 25:9, 10
Yer 39:8i 2Fa 22:16, 17
Omb 4:11

SURA YA 18

j Yer 19:1

Yerusalemu;^a na jiji hili litae-ndelea kuwa na watu daima.

26 Na watu watakuja kutoka katika majiji ya Yuda, kutoka maeneo yanayozunguka Yerusalemu, kutoka nchi ya Benjamin,^b maeneo ya chini,^c kutoka eneo lenye milima, na kutoka Negebu;^{*} wataleta dhabihu nzima za kuteketezwa,^d dhabihu nyingine,^e matoleo ya nafaka,^f ubani, na dhabihu za shukrani ndani ya nyumba ya Yehova.^g

27 ““Lakini msiponitii kwa kutoshika siku ya Sabato ikiwa siku takatifu na mkibeba mizigo na kuileta kupitia malango ya Yerusalemu katika siku ya Sabato, nitayawasha moto malango yake, nao hakika utaiteketeza minara yenye ngome ya Yerusalemu^h nao hautazimwa.”ⁱ

18 Hili ndilo neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova: **2** “Inuka na ushuke mpaka kwenye nyumba ya mfinyanzi,^j na huko nitakuaambia maneno yangu.”

3 Basi nikashuka mpaka kwenye nyumba ya mfinyanzi, naye alikuwa akifanya kazi kwenye magurudumu ya mfinyanzi. **4** Lakini chombo alichokuwa akitengeneza kika-haribika mikononi mwake. Basi mfinyanzi akakitengeneza upya kuwa chombo kingine, kama alivyopenda.*

5 Kisha neno la Yehova likanjia likisema: **6** “Je, siwezi kuwatendea kama mfinyanzi huyu alivyotenda, enyi watu wa nyumba ya Israeli?” asema Yehova. “Tazama! Kama udongo mikononi mwa mfinyanzi,

17:26 *Au “kusini.” 18:4 *Tnn., “kama ilivyokuwa sawa machoni pa mfinyanzi kukitengeneza.”

ndivyo mlivyo mikononi mwangu, enyi watu wa nyumba ya Israeli.^a **7** Wakati wowote nitakaposema kuhusu kung'oa na kubomoa na kuharibu taifa au ufalme,^b **8** na taifa hilo liache uovu wake niliotangaza dhidi yake, mimi pia nitabadili nia yangu* kuhusu msiba niliokusudia kuuleta dhidi yake.^c **9** Lakini wakati wowote ninaposema kuhusu kujenga na kupanda taifa au ufalme, **10** na taifa hilo litende maovu machoni pangu na kukosa kuitii sauti yangu, mimi pia nitabadili nia yangu* kuhusu mema niliyokusudia kulitendea.'

11 "Sasa, tafadhali, wambie watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu, 'Yehova anasema hivi: "Ninatayarisha* msiba na kupanga njama dhidi yenu. Geukeni, tafadhali, kutoka kwenye njia zenu mbaaya, na mrekebishe njia zenu na matendo yenu."'''^d

12 Lakini wakasema: "Hakuna tumaini lolote!^e Kwa maana tutafuata mawazo yetu wenyewe, na kila mmoja wetu atatenda kulingana na ukaidi wa moyo wake mwovu."^f

13 Kwa hiyo Yehova anasema hivi:

"Ulizeni wenyewe, tafadhali, kati ya mataifa. Ni nani amesikia jambo kama hili?

Bikira wa Israeli ametenda jambo linalochukiza sana.^g

14 Je, teluji ya Lebanoni inatoweka kwenye miamba iliyo kwenye miteremko yake?

18:8, 10 *Au "nitaghairi." 18:11 *Tnn., "ninatengeneza."

SURA YA 18

a Ro 9:20, 21

b Yer 1:10
Yer 12:14
Yer 25:9
Yer 45:4

c 1Fa 8:33, 34
Zb 106:45
Yer 7:3
Yer 26:3
Eze 18:21
Yoe 2:13
Yon 3:5, 10

d Isa 1:16
Eze 18:23

e Yer 2:25

f Kum 29:19, 20
Yer 7:24

g Yer 2:13

Safu ya 2

a Yer 2:19
Yer 3:21

b Yer 10:14, 15

c Yer 6:16

d Law 26:33
Eze 6:14

e 1Fa 9:8
Yer 19:8
Omb 2:15
Mik 6:16

f Kum 28:37

g Kum 31:17

h Yer 11:19

Au, je, maji baridi yanayotiririka kutoka mbali yatakauka?

15 Lakini watu wangu wamenisahau.^a

Kwa maana wanakitolea dhabihu* kitu cha ubatili,^b

Nao wanawafanya watu wajikwae katika njia zao, vijia vya kale,^c

Ili wapite kwenye barabara za vichochoroni ambazo hazijasawazishwa na ambazo si tambarare,[#]

16 Ili kuifanya nchi yao kuwa kitu cha kutisha^d

Na kitu cha kupigiwa mluzi milele.^e

Kila mtu atakayepita kando yake atatazama kwa mshtuko na kutikisa kichwa chake.^f

17 Kama upepo wa mashariki, nitawatawanya mbele ya adui.

Nitawaonyesha mgongo, si uso wangu, siku ya msiba wao."^g

18 Nao wakasema: "Njooi, tupange njama dhidi ya Yere-mia,^h kwa maana sheria haitatoweka* kutoka kwa makuhani wetu au shauri kutoka kwa watu wenye hekima au neno kutoka kwa manabii. Njooi tumshambulie kwa maneno,[#] nasi tusisikilize anachosema."

19 Nitegee sikio, Ee Yehova, Nawe usikilize wanachosema wapinzani wangu.

20 Je, wema unapaswa kuli-pwa kwa uovu?

18:15 *Au "moshi wa dhabihu." #Au "ambazo hazijatengenezwa." 18:18 *Au "mafundisho hayatatoweka." #Tnn., "tumpige kwa ulimi."

Kwa maana wameuchimbia shimo uhai wangu.*^a

Kumbuka jinsi nilivyosi-mama mbele zako ili kusema mema kuwahusu,

Ili kuwaondolea ghadhabu yako.

- 21** Basi waache wana wao wapwatwe na njaa kali, Na uwatie mikononi mwa nguvu za upanga.^b Wake zao na wafiwe na watoto na kuwa wajane.^c Wanaume wao na wauawe kwa ugonjwa unaoua, Vijana wao wauawe kwa upanga vitani.^d

- 22** Kilio na kisikiwe kutoka katika nyumba zao Utakapowaletea wavamizi kwa ghafla.

Kwa maana wamechimbia shimo ili kunikamata Nao wametega mitego ya kuinasa miguu yangu.^e

- 23** Lakini wewe, Ee Yehova, Unajua vema njama zao zote za kuniua.^f Usilifunike kosa lao, Wala usifute dhambi yao kutoka mbele zako. Na wakwazike mbele zako^g Utakapowachukulia hatua kwa hasira yako.^h

19 Yehova alisema hivi: “Nenda ukanunue chupa ya udongo kwa mfinyanzi.ⁱ Uwachukue baadhi ya wazee wa watu na baadhi ya wazee wa makuhani, **2** nawe uende katika Bonde la Mwana wa Hinomu,^j kwenye njia inayoelekea kwenye Lango la Viga. Na huko utangaze mane-

18:20 *Au “wameichimbia shimo nafsi yangu.”

SURA YA 18

a Zb 35:7

b Yer 12:3

c Omb 5:3

d 2Nya 36:17

e Zb 38:12

f Yer 11:19, 20

g Zb 35:4

h Yer 15:15

SURA YA 19

i Yer 18:2

j Yos 15:8, 12
2Nya 28:1, 3
Yer 7:31

Safu ya 2

a 2Fa 22:16, 17
Isa 65:11

b 2Nya 33:1, 4

c 2Fa 21:16
Isa 59:7
Yer 2:34
Omb 4:13
Mt 23:34, 35

d 2Nya 28:1, 3
2Nya 33:1, 6
Isa 57:5

e Law 18:21
Yer 7:31
Yer 32:35

f Yer 7:32

g Kum 28:25, 26
Zb 79:2
Yer 7:33
Yer 16:4

no ninayokuambia. **3** Utasema, ‘Sikieni neno la Yehova, enyi wafalme wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu. Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi:

““Niko karibu kuleta msiba mahali hapa, na masikio ya yeyote anayesikia kuuhusu yatawasha. **4** Ni kwa sababu waliniacha^a na kufanya mahali hapa pasitambuliwe.^b Hapa wanaitolea dhabihu miungu mingine ambayo wao na mababu zao na wafalme wa Yuda hawakuijua, nao wamepajaza mahali hapa damu ya watu wasio na hatia.^c **5** Walijenga mahali pa juu pa Baali ili kuwateketeza motoni wana wao kuwa dhabihu nzima za kuteketezwa kwa Baali,^d jambo ambalo sikuamuru wala kusema na ambalo hata halijawahi kamwe kuingia moyoni mwangu.”^e

6 ““Kwa hiyo tazameni! siku zinakuja,” asema Yehova, “wakati mahali hapa hapataitwa tena Tofethi au Bonde la Mwana wa Hinomu bali Bonde la Mauaji.^f **7** Nitavunja mipango ya Yuda na Yerusalemu mahali hapa, nami nitawaacha maadui wao wawaangamize kwa upanga na pia wataangamizwa kwa mkono wa wale wanaotaka kuwaua.* Nami nitawapa ndege wa angani na wanyama wa duniani maiti zao kuwa chakula chao.^g **8** Nitalifanya jiji hili kuwa kitu cha kutisha na kitu cha kupigiwa mluzi. Kila mtu atakayepita kando yake atatazama kwa mshtuko na kupiga mluzi kwa sababu ya mapigo

19:5 *Au “sijawahi kamwe kulifikiria.”
19:7 *Au “wanaotafuta nafsi yao.”

yake yote.^a **9** Nami nitawafanya wale nyama ya wana wao na ya mabinti wao, nao watakuwa kila mmoja nyama ya mwenzake, kwa sababu ya kuzingirwa na kukata tamaa watakapobanwa na maadui wao wanaotaka kuwaua.”^{*b}

10 “Kisha uivunje ile chupa mbele ya macho ya wanaume watakaenda pamoja nawe, **11** nawe uwaambie, ‘Yehova wa majeshi anasema hivi: “Hivi ndivyo nitakavyovavunja watu hawa na jiji hili, kama mtu anavyovunja chombo cha mfinyanzi hivi kwamba hakiwezi kurekebishwa kamwe; nao watawazika wafu katika Tofethi hivi kwamba hakutakuwa na nafasi zaidi ya kuwazika.”^c

12 “Hivyo ndivyo nitakavyopatendea mahali hapa,’ asema Yehova, ‘na wakaaji wake, ili kulifanya jiji hili liwe kama Tofethi. **13** Na nyumba za Yerusalemu na nyumba za wafalme wa Yuda zitakuwa chafu kama mahali hapa, Tofethi,^d naam, nyumba zote ambazo juu ya paa zake walilitolea dhabihu jeshi lote la mbinguni^e na ambako walimimimia miungu mingine matoleo ya kinywaji.”^f

14 Yeremia aliporudi kutoa Tofethi ambako Yehova alikuwa amemtuma ili atabiri huko, akasimama katika ua wa nyumba ya Yehova na kuwaambia hivi watu wote: **15** “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Tazameni, ninaliletea jiji hili na miji yake yote msiba wote ambao nimetangaza dhidi yake, kwa sababu walika-

19:9 *Au “wanaotafuta nafsi yao.”

SURA YA 19

a 1Fa 9:8
Yer 18:16
Omb 2:15

b Law 26:29
Kum 28:53
Omb 4:20
Omb 4:10
Eze 5:10

c Yer 7:32

d Zb 79:1

e Yer 8:1, 2
Sef 1:4, 5

f Yer 7:18
Yer 32:29

Safu ya 2

a Ne 9:17, 29
Zek 7:12

SURA YA 20

b 2Nya 16:10

c Yer 6:25

d Kum 28:32

e Yer 25:9
Yer 39:9

f 2Fa 20:17
2Fa 24:11, 13
2Fa 25:13-15
Omb 1:10

g 2Nya 36:10
Yer 15:13

h Yer 14:14
Yer 28:15
Yer 29:21

taa kwa ukaidi kuyatii* mane-no yangu.”^a

20 Sasa Pashuri mwana wa Imeri, kuhani, ambaye pia alikuwa msimamizi mkuu katika nyumba ya Yehova, alikuwa akisikiliza Yeremia alipokuwa akitabiri mambo hayo. **2** Kisha Pashuri akampiga nabii Yeremia na kumweka katika mikatale^b iliyo kuwa kwenye Lango la Juu la Benjamini, lililokuwa katika nyumba ya Yehova. **3** Lakini siku iliyofuata Pashuri alipomtoa Yeremia katika ile mikatale, Yeremia akamwambia:

“Yehova hatakuita tena Pashuri, bali Hofu Kila Upande.^c

4 Kwa maana Yehova anasema hivi: ‘Nitakufanya uwe kitu cha kutia hofu kwako mwenyewe na kwa marafiki wako wote, nao watauawa kwa upanga wa maadui wao huku macho yako yakitazama;^d nami nitawatia watu wote wa Yuda mikononi mwa mfalme wa Babiloni, naye atawapeleka uhamishoni kule Babiloni na kuwaua kwa upanga.^e **5** Nami nitatia mikononi mwa maadui wao utajiri wote wa jiji hili, mali zake zote, vitu vyake vyote vyenye thamani, na hazina zote za wafalme wa Yuda.^f Nao watapora vitu hivyo na kuvichukua na kuvipeleka Babiloni.^g **6** Lakini wewe, Pashuri, na wote wanaoishi katika nyumba yako, mtapelekwa utekwani. Utapelekwa Babiloni na kufia huko, nawe utazikwa huko pamoja na marafiki wako wote, kwa sababu ume-watabiria uwongo.”^h

19:15 *Tnn., “walizifanya shingo zao kuwa ngumu ili wasitii.”

- 7** Umenipumbaza, Ee Yehova, nami nikapumbazika. Ulizitumia nguvu zako kunipinga, nawe uka-shinda.^a
Nimekuwa kitu cha kuche-kwa mchana kutwa;
Kila mtu ananidhihaki.^b
- 8** Kwa maana kila mara ninapozungumza, lazima nipaze sauti na kutangaza,
“Ukatili na uharibifu!”
Kwa maana neno la Yehova limesababisha nitukane na kudhihakiwa siku nzima.^c
- 9** Basi nikasema: “Sitamtaja tena,
Wala sitasema tena katika jina lake.”^d
Lakini moyoni mwangu neno hilo lilikuwa kama moto unaowaka uliofungiwa mifupani mwangu, Nami nikachoka kulizuia ndani yangu;
Singeweza tena kuvumilia.^e
- 10** Kwa maana nilisikia uvumi mwingi wa uovu; Hofu ilinizunguka.^f
“Mshutumuni; na tumshutumuni!”
Kila mtu aliyenitakia amani alisubiri nianguke.^g
“Labda atafanya kosa la kipumbavu,
Nasi tutamshinda na kujilipizia kisasi dhidi yake.”
- 11** Lakini Yehova alikuwa pamoja nami kama shujaa anayetisha.^h
Ndiye sababu wale wanaonitesa watajikwaa nao hawatashinda.ⁱ
Wataaibishwa sana, kwa maana hawatafanikiwa.

SURA YA 20

a Eze 3:14
Mik 3:8

b Zb 22:7
Yer 15:10, 15

c 2Nya 36:16
Yer 6:10

d 1Fa 19:2, 4
Yon 1:3

e Yer 6:11
Amo 3:8
Mdo 4:19, 20

f Zb 31:13

g Zb 38:16

h Yer 1:8
Ro 8:31

i Zb 27:2
Yer 15:15, 20
Yer 17:18

Safu ya 2

a Zb 6:10

b Yer 17:10

c Zb 59:10
Yer 17:18

d Yer 11:20
1Pe 2:23

e Ayu 3:3
Yer 15:10

f Ayu 10:18

g Ayu 3:20

Fedheha yao ya milele haitasahauliwa.^a

- 12** Lakini wewe, Ee Yehova wa majeshi, unamchu-nguza mwadilifu;
Unaona mawazo ya ndani kabisa* na pia moyo.^b
Acha nione ukiwalipiza kisasi,^c
Kwa maana nimeileta kesi yangu kwako.^d
- 13** Mwimbieni Yehova! Msifuni Yehova!
Kwa maana amemwoko maskini* kutoka mikoni mwa watenda maovu.
- 14** Ilaaniwe siku niliyojaliwa! Isibarikiwe siku ambayo mama yangu alinizaa!^e
- 15** Alaaniwe mtu aliyemletea baba yangu habari nje-ma, akisema:
“Umepata mwana, mvulana!”
Na kumfanya ashangilie sana.
- 16** Mtu huyo na awe kama majiji ambayo Yehova aliyaangamiza bila ku-ghairi.
Na asikie kilio asubuhi na sauti ya king'ora adhuri.
- 17** Kwa nini hakuniua ndani ya tumbo la uzazi,
Ili mama yangu awe kaburi langu
Na tumbo lake liwe na mimba sikuzote?^f
- 18** Kwa nini nilitoka tumboni Ili kuona taabu na huzuni, Na kumaliza siku zangu kwa aibu?^g

20:12 *Au “hisia za ndani kabisa.” Tnn., “figo.” 20:13 *Au “ameiokoa nafsi ya maskini.”

21 Yeremia alipokea neno kutoka kwa Yehova wakati Mfalme Sedekia^a alipomtuma kwake Pashuri^b mwana wa Malkiya na Sefania^c mwana wa Maaseya, kuhani, akionamba hivi: **2** “Tafadhali mwombe Yehova ushauri kwa ajili yetu, kwa sababu Mfalme Nebukadnezar^{*} wa Babiloni anapigana vita dhidi yetu.^d Labda Yehova atatutendea mojawapo ya matendo yake yanayostajibisha, ili mfalme huyo atuche na kwenda zake.”^e

3 Yeremia akawaambia, “Mwambieni Sedekia hivi: **4** ‘Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: “Tazama, ninazigeuza dhidi yenu^{*} silaha za vita zilizo mikononi mwenu, mnaotumia kupigana na mfalme wa Babiloni^f na Wakaldayo wanaowazingira nje ya ukuta. Nami nitawakusanya katikati ya jiji hili. **5** Na mimi mwenyewe nitapigana nanyi^g kwa mkono ulionyooshwa na kwa mkono wenye nguvu, kwa hasira na kwa ghadhabu na kwa ukali mwingi.^h **6** Nitawapiga wakaaji wa jiji hili, mwanadamu na mnyama pia. Watakufa kwa ugonjwa hatari sana.”ⁱ

7 ““Baada ya hayo,” asema Yehova, “Nitamtia Mfalme Sedekia wa Yuda na watumishi wake na watu wa jiji hili—wale watakaookoka ugonjwa hatari, upanga, na njaa kali—mikononi mwa Mfalme Nebukadnezar^{*} wa Babiloni, mikononi mwa maadui wao na mikononi mwa wale wanaotaka kuwaua.^{#j} Atawaua kwa upanga.

21:2, 7 *Tnn., “Nebukadrezar,” njia nyingine ya kuandika jina hili. **21:4** *Au “ninawageuzia.” **21:7** *Au “wanaotafuta nafsi yao.”

SURA YA 21

a 2Fa 24:18
1Nya 3:15
2Nya 36:9, 10

b Yer 38:1

c Yer 29:25
Yer 37:3
Yer 52:24, 27

d 2Fa 25:1
Yer 32:28
Yer 39:1

e 1Sa 7:10
2Nya 14:11
Isa 37:36, 37

f Yer 32:5

g Isa 63:10
Omb 2:5

h Isa 5:25

i Kum 28:21, 22
Eze 7:15

j 2Fa 25:6, 7
Yer 37:17
Yer 39:5-7
Yer 52:9-11
Eze 17:20

Safu ya 2

a Kum 28:49, 50
2Nya 36:17

b Yer 27:12, 13
Yer 38:2, 17

c Yer 44:11

d Yer 38:3

e 2Nya 36:17, 19
Yer 17:27
Yer 34:2
Yer 37:10
Yer 39:8

f Isa 1:17
Yer 22:3
Eze 22:29
Mik 2:2

g Kum 32:22
Isa 1:31
Yer 7:20

h Yer 7:5-7

Hatawasikitikia wala kuwahurumia wala kuwaonyesha rehema yoyote.”^a

8 “Nawe utawaambia watu hawa, ‘Yehova anasema hivi: “Tazameni, ninaweka mbele yenu njia ya uzima na njia ya kifo. **9** Wale watakaobaki katika jiji hili watakufa kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari. Lakinii yeyote atakayetoka na kujisalimisha kwa Wakaldayo wanaowazingira ataendelea kuishi, naye atapata uhai wake^{*} kama nyara.”^{#b}

10 ““Kwa maana nimelika-taa^{*} jiji hili nalo litapata msiba wala si mema,”^c asema Yehova. “Litatiwa mikononi mwa mfalme wa Babiloni,^d naye ataliteketeza kwa moto.”^e

11 ““Utawaambia watu wa nyumba ya mfalme wa Yuda: Sikieni neno la Yehova. **12** Enyi watu wa nyumba ya Daudi, Yehova anasema hivi:

“Tekelezeni haki kila asubuhi,

Na mtu anayenyang’anywa, mwokoeni kutoka mikononi mwa mtu la-ghai,^f

Ili ghadhabu yangu isiwake kama moto^g

Na kuteketeza bila mtu wa kuuzima

Kwa sababu ya matendo yenu maovu.”^h

13 “Tazama, niko dhidi yako, ewe mkaaji wa bondeni,^{*} Ewe mwamba wa nchi tamarbarare,^{*} asema Yehova. ‘Na wewe unayeuliza:

21:9 *Au “nafsi yake.” #Au “ataponyoka na uhai wake.” **21:10** *Tnn., “nimeukaza uso wangu dhidi ya.” **21:13** *Au “nchi tamarbarare ya chini.”

“Ni nani atakayeshuka kupigana nasi?

Na ni nani atakayevamia makao yetu?”

14 Nitakufanya uwajibike*

Kulingana na matendo yenu,^a asema Yehova.

“Nami nitawasha moto katika msitu wake,

Nao utateketeza vitu vyote vinavyomzunguka.”^b

22 Yehova anasema hivi:

“Shuka nyumbani kwa* mfalme wa Yuda, upeleke ujumbe huu. **2** Utasema, ‘Sikia neno la Yehova, ewe mfalme wa Yuda unayeketi juu ya kiti cha ufalme cha Daudi, wewe pamoja na watumishi wako na watu wako, wale wanaoingia kupitia malango haya. **3** Yehova anasema hivi: “Tekelezeni haki na uadilifu. Na mtu anayenyang’anywa, mwokoeni kutoka mikononi mwa mtu laghai. Msimtese mkaaji yeyote mgeni, na msimduru yatima yeyote au mjane.^c Nanyi msimwage damu yoyote isiyo na hatia mahali hapa.^d **4** Kwa maana mkijitahidi kufuata neno hili, basi wafalme wanaoketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi^e wataingia kupitia malango ya nyumba hii, wakiwa wamepanda magari na farasi, wao pamoja na watumishi wao na watu wao.”^f

5 “Lakini msipoyatii maneno haya, ninaapa kwa nafsi yangu mwenyewe,’ asema Yehova, ‘kwamba nyumba hii itakuwa ukiwa.’^g

6 “Kwa maana Yehova anasema hivi kuhusu nyumba ya mfalme wa Yuda,

21:14 *Au “Nitakuadhibu.” 22:1 *Au “kwenye jumba la kifalme la.”

SURA YA 21

a Yer 5:9
Yer 9:9

b 2Nya 36:17, 19
Yer 52:12, 13

SURA YA 22

c Law 19:15
Isa 1:17
Eze 22:7
Mik 2:2

d 2Fa 24:3, 4
Yer 7:6, 7

e 1Fa 2:12

f Yer 17:24, 25

g Yer 39:8
Mik 3:12

Safu ya 2

a Isa 6:11
Yer 7:34

b Eze 9:1

c Yer 21:14

d Kum 29:24–26
1Fa 9:8, 9
Omb 2:15

e 2Fa 22:16, 17

f 1Nya 3:15
2Nya 36:1

g 2Fa 23:29, 30

h 2Fa 23:34
2Nya 36:4

‘Wewe ni kama Gileadi kwangu,
Kama kilele cha Lebanoni.
Lakini nitakufanya uwe nyika;

Hakuna jiji lako hata moja litakalokaliwa.^a

7 Nami nitawaweka* waangamizaji dhidi yako,
Kila mmoja akiwa na silaha zake.^b

Wataikata mierezi yako iliyo bora zaidi

Na kuangusha ndani ya moto.^c

8 Na mataifa mengi yatapita kando ya jiji hili na kila mmoja atamwambia mwenzake: “Kwa nini Yehova alilitendea hivi jiji hili kuu?”^d

9 Nao watajibu: “Kwa sababu waliliacha agano la Yehova Mungu wao na kuiinamia miungu mingine na kuitumikia.”^e

10 “Msimlilie aliyekufa,
Na msimsikitikie.

Badala yake, mlilieni sana yule anayeondoka,
Kwa maana hatarudi tena kuiona nchi alimozaliwa.

11 “Kwa maana Yehova anasema hivi kumhusu Shalumu*^f mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda anayetawala badala ya Yosia^g baba yake, ambaye ameondoka mahali hapa: ‘Hatarudi hapo tena. **12** Kwa maana atakufa mahali walipompeleka uhamishoni, naye hataiona tena nchi hii.’^h

13 Ole wake anayejenga nyumba yake bila uadilifu
Na vyumba vyake vya juu bila haki,
Anayemfanya mwana-

22:7 *Tnn., “nitawatakasa.” 22:11 *Pia anaitwa Yehoahazi.

- damu mwenzake
amtumikie bure,
Na ambaye anakataa ku-
mlipa malipo yake;^a
- 14** Yule anayesema, 'Nitaji-
jengea nyumba yenye
nafasi kubwa
Yenye vyumba vya juu
vyenye nafasi kubwa.
Nitaiwekea madirisha
Nami nitazifunika kuta
zake kwa mbao za mie-
rezi na kuipaka rangi
nyekundu.'
- 15** Je, utaendelea kutawala
kwa sababu unawashi-
nda wengine kwa
kutumia mierezi?
Baba yako pia alikula na
kunywa,
Lakini alitenda haki na ua-
dilifu,^b
Naye alifanikiwa.
- 16** Alitetea haki halali ya
mwenye kuteseka na ma-
skini,
Basi akafanikiwa.
'Hiyo ndiyo maana ya
kunijua, sivyo?' asema
Yehova.
- 17** 'Lakini macho yako na
moyo wako unakazia tu
faida yako isiyo ya haki,
Kumwaga damu isiyo na
hatia,
Na kufanya ulaghai na
unyang'anyi.'
- 18** "Kwa hiyo Yehova anase-
ma hivi kumhusu Yehoyaki-
mu^c mwana wa Yosia, mfalme wa
Yuda,
'Hawatamwombolezea:
"Aa! ndugu yangu! Aa!
dada yangu!"
Hawatamwombolezea:
"Aa! Ewe bwana! Aa! mfa-
lme!"

SURA YA 22

a Law 19:13
Mik 3:9, 10

b 2Fa 22:1, 2
2Fa 23:23, 25

c 2Fa 23:34
2Nya 36:4

Safu ya 2

a Yer 36:30

b 2Nya 36:5, 6

c Kum 32:49

d 2Fa 24:7

e Yer 2:31
Yer 6:16

f Kum 9:7
Amu 2:11

g Yer 23:1
Eze 34:2

h Yer 22:6

i Isa 2:12, 13

j Yer 4:31
Yer 6:24

k 2Fa 24:6
Yer 22:28
Yer 37:1
Mt 1:11

l 2Fa 23:34

- 19** Atazikwa kama anavyozi-
kwa punda,^a
Kwa kukokotwa na ku-
tupwa,
Nje ya malango ya Yerusa-
lemu.^b
- 20** Panda mpaka Lebanoni na
upaze kilio,
Paza sauti yako huko Ba-
shani.
Na upaze kilio kutoka Aba-
rimu,^c
Kwa maana wapenzi wako
wamepondwa.^d
- 21** Nilisema nawe ulipokuwa
salama.
Lakini ulisema, 'Sitatii.'^e
Hii imekuwa njia yako ta-
ngu ujana wako,
Kwa maana hujaitii sauti
yangu.^f
- 22** Upepo utawachunga wa-
chungaji wako wote,^g
Na wapenzi wako watae-
nda utekwani.
Kisha utaaibishwa na kufe-
dheheshwa kwa sababu
ya msiba wako wote.
- 23** Ewe unayekaa Lebanoni,^h
Uliye na kiota kati ya mie-
rezi,ⁱ
Jinsi utakavyougua uchu-
ngu utakapokupata,
Maumivu* kama ya mwa-
namke anayezaa!"^j
- 24** "Kwa hakika kama nina-
vyoishi,' asema Yehova, 'hata
kama Konia*^k mwana wa Ye-
hoyakimu,^l mfalme wa Yuda,
angekuwa pete ya muhuri
kwenye mkono wangu wa
kuume, ningekung'oa kuto-
ka hapo! **25** Nami nitaku-
tia mkononi mwa wale wanao-
taka kukuua,* mkononi mwa

22:23 *Tnn., "Uchungu wa kuzaa."

22:24 *Pia anaitwa Yehoyakini na Ye-
konia. 22:25 *Au "wanaotafuta nafsi
yako."

wale unaowaogopa, mkononi mwa Mfalme Nebukadnereza* wa Babiloni, na mkononi mwa Wakaldayo.^a **26** Nami nitakutupa wewe pamoja na mama yako aliyekuzaa katika nchi nyingine ambako hamkuzaliwa, nanyi mtakufa huko. **27** Nao hawatarudi kamwe katika nchi wanayoitamani.*^b

28 Je, mtu huyu Konia ni chungu tu kilichodhauruliwa na kuvunjika, Chombo ambako hakuna mtu anayekitaka?

Kwa nini yeye na wazao wake wameangushwa chini

Na kutupwa katika nchi wasiyoiujua?^c

29 Ewe dunia,* dunia, dunia, sikia neno la Yehova.

30 Yehova anasema hivi:

'Andikeni kwamba mtu huyu hana mtoto, Kama mtu ambaye hatafanikiwa katika maisha yake,*

Kwa maana hakuna yeyote kati ya wazao wake atakayefanikiwa

Kuketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi na kutawala tena katika Yuda."^d

23 "Ole wao wachungaji wanaowaangamiza na kuwatawanya kondoo wa malisho yangu!" asema Yehova.^e

2 Kwa hiyo Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi dhidi ya wachungaji wanaowachunga watu wangu: "Mmewatawanya kondoo wangu; mlie-

22:25 *Tnn., "Nebukadreza," njia nyingine ya kuandika jina hili. **22:27** *Au "kwenye nchi ambayo wanaiinulia nafsi yao." **22:29** *Au "nchi." **22:30** *Tnn., "siku zake."

SURA YA 22

a 2Fa 24:12, 15
2Nya 36:9, 10
Yer 24:1
Yer 29:1, 2

b Yer 52:31-34

c 1Nya 3:17, 18

d 2Nya 36:9, 10
Yer 36:30
Mt 1:12

SURA YA 23

e Yer 10:21
Yer 50:6
Eze 34:2

Safu ya 2

a Eze 34:5

b Isa 11:11
Isa 35:10
Yer 29:14
Yer 31:8

c Yer 50:19
Eze 34:14
Mik 2:12

d Kum 30:3, 5
Amo 9:14
Zek 10:8

e Yer 3:15
Yoh 21:15
Mdo 20:28

f Isa 11:1
Isa 53:2
Yer 33:15, 16
Zek 3:8
Mt 2:23

g Lu 1:32, 33

h Isa 9:7
Isa 11:3, 4
Isa 32:1

i Zek 10:6

j Kum 33:28
Yer 32:37
Zek 14:11

k Isa 54:17

l Yer 16:14, 15

m Isa 43:5
Eze 34:13
Sef 3:20

ndelea kuwatawanya, nanyi hamjawakazia fikira."^a

"Basi nitawakazia ninyi fikira kwa sababu ya matendo yenu maovu," asema Yehova.

3 "Kisha nitawakusanya kondoo wangu waliobaki kutoka katika nchi zote ambako nilikuwa nimewatawanya,^b nami nitawarudisha kwenye malisho yao,^c nao watazaana na kuwa wengi.^d **4** Nami nitaweka wachungaji juu yao ambao kwa kweli watawachunga.^e Hawataogopa tena wala kuwa na hofu, na hakuna yeyote atakayekosekana," asema Yehova.

5 "Tazameni! Siku zinakuja," asema Yehova, "nitakapomwinulia Daudi chipukizi adilifu.*^f Na mfalme atatawala^g na kuwa na ufahamu na kutekeleza haki na uadilifu katika nchi.^h **6** Katika siku zake Yuda ataokolewa,ⁱ na Israeli atakaa kwa usalama.^j Naye ataitwa jina hili: Yehova Ni Uadilifu Wetu."^k

7 "Hata hivyo, siku zinakuja," asema Yehova, "wakati ambapo hawatasesema tena, 'Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, aliyewatoa watu wa Israeli nchini Misri!'^l **8** badala yake watasema, 'Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, aliyewatoa na kuwarudisha wazao wa nyumba ya Israeli kutoka katika nchi ya kaskazini na kutoka katika nchi zote nilizowatawanya,' nao watakaa katika nchi yao wenyewe."^m

9 Kuhusu manabii:

Moyo wangu umevunjika ndani yangu.

Mifupa yangu yote inatetemeka.

23:5 *Au "mrithi mwadilifu."

Mimi ni kama mtu aliyelewa

Na kama mtu aliyelemewa na divai,

Kwa sababu ya Yehova na kwa sababu ya maneno yake matakatifu.

10 Kwa maana nchi imejaa wazinzi;^a

Kwa sababu ya laana nchi inaomboleza^b

Na malisho ya nyikani yamekauka.^c

Njia yao ni ya uovu, nao wanatumia vibaya nguvu zao.

11 “Nabii pamoja na kuhani wamechafuliwa.”^{*d}

Hata katika nyumba yangu mwenyewe nimeupata uovu wao,^e asema Yehova.

12 “Basi kijia chao kitakuwa na utelezi na giza,^f Watasukumwa na kuanguka.

Kwa maana nitawaletea msiba

Katika mwaka wa kuwadhibu,” asema Yehova.

13 “Na kwa manabii wa Samaria^g nimeona jambo linalochukiza sana.

Unabii wao unachochea na Baali,

Nao wanawapotosha watu wangu Waisraeli.

14 Na kwa manabii wa Yerusalemu nimeona mambo mabaya sana.

Wanafanya uzinzi^h na kutembea katika uwongo;ⁱ Wanawatia moyo^{*} watenda maovu,

Nao hawageuki na kuacha uovu wao.

23:11 *Au “wameasi imani.” 23:14 *Tnn., “Wanaitia nguvu mikono ya.”

SURA YA 23

a Yer 3:8, 9
Yer 5:7
Yer 13:27
Eze 22:11

b Isa 24:4
Yoe 1:10

c Yer 12:4

d Isa 28:7
Yer 5:31
Yer 6:13
Eze 22:25
Sef 3:4

e 2Nya 33:1, 5
2Nya 36:14
Yer 7:11
Eze 8:10, 11
Eze 23:39

f Yer 13:16

g Eze 16:46

h Yer 29:21, 23

i Yer 23:26

Safu ya 2

a Isa 3:9

b Mwa 18:20
Kum 32:32
Isa 1:10
Yud 7

c Yer 8:14
Yer 9:15

d Yer 27:9
Yer 29:8

e Omb 2:14

f Yer 14:14
Eze 13:3
Eze 22:28

g Yer 4:10
Yer 6:13, 14
Yer 8:11
Eze 13:10

h Mik 3:11

Wote ni kama Sodoma kwangu,^a

Na wakaaji wake ni kama Gomora.”^b

15 Kwa hiyo Yehova wa majeshi anasema hivi dhidi ya manabii hao:

“Tazama, ninawafanya wale pakanga

Na kuwapa maji yenye sumu wanywe.^c

Kwa maana kutoka kwa manabii wa Yerusalemu uasi imani umeenea katika nchi yote.”

16 Yehova wa majeshi anasema hivi:

“Msiyasikilize maneno ya manabii wanaowatabiria ninyi.^d

Wanawadanganya.*

Wanasema maono ya moyo wao wenyewe,^e

Si kutoka katika kinywa cha Yehova.^f

17 Wanawaambia tena na tena wale wasionihe-shimu,

‘Yehova amesema hivi: “Mtakuwa na amani.”’^g

Nao wanamwambia kila mtu anayefuata moyo wake mkaidi,

‘Hutapatwa na msiba wote.’^h

18 Kwa maana ni nani amesimama katika kikundi cha marafiki wa karibu wa Yehova

Ili aone na kulisikia neno lake?

Ni nani amelikazia fikira neno lake ili alisikie?

19 Tazameni! Dhoruba ya upepo ya Yehova italipuka kwa ghadhabu;

23:16 *Au “Wanawajaza matumaini ya uwongo.”

Kama tufani inayozunguka, itazunguka ikishuka juu ya kichwa cha waovu.^a

20 Hasira ya Yehova haitapoa Mpaka atakapoteketeleza na kutimiza makusudi ya moyo wake.

Mtaelewa jambo hilo waziwazi katika siku za mwisho.

21 Sikuwatuma manabii, lakini waliikimbia.

Sikuongea nao, lakini wali-tabiri.^b

22 Lakini ikiwa wangesima katika kikundi changu cha marafiki wa karibu,

Wangewafanya watu wangu wayasikie maneno yangu

Nao wangewarudisha kutoka kwenye njia yao mbaya na matendo yao maovu.^c

23 "Je, mimi ni Mungu nikiwa karibu tu," auliza Yehova, "na si Mungu nikiwa mbali pia?"

24 "Je, mtu yeyote anaweza kujificha mahali pa siri ambapo siwezi kumwona?"^d auliza Yehova.

"Je, mimi sizijazi mbingu na dunia?"^e auliza Yehova.

25 "Nimewasikia manabii wanaotabiri uwongo katika jina langu wakisema, 'Niliota ndoto! Niliota ndoto!'^f **26** Jambo hili litaendelea mpaka lini katika moyo wa manabii hao, kutabiri uwongo? Wao ni manabii wa udanganyifu wa moyo wao wenyewe.^g **27** Wanakusudia kuwafanya watu wangu walisahau jina langu kupitia ndoto

SURA YA 23

a Yer 25:32
Yer 30:23, 24

b Yer 14:14
Yer 27:15
Yer 29:8, 9

c Yer 25:4, 5

d Mwa 16:7, 13
Met 15:3
Amo 9:2
Ebr 4:13

e Zb 139:7

f Kum 18:20
Yer 27:9
Yer 29:21, 23

g Yer 14:14

Safu ya 2

a Amu 3:7
2Fa 21:1, 3

b Yer 5:14

c Ebr 4:12

d Kum 18:20
Yer 14:15
Eze 13:2, 3

e Eze 13:7

f Sef 3:4

g Yer 7:8
Omb 2:14

h Yer 12:7

wanzosimuliana, kama baba zao walivyolisahau jina langu kwa sababu ya Baali.^a **28** Nabii aliye na ndoto na asimulie ndoto hiyo, lakini yule aliye na neno langu anapaswa kulisema neno langu kwa ukweli."

"Nyasi ina uhusiano gani na nafaka?" auliza Yehova.

29 "Je, neno langu si kama moto,"^b auliza Yehova, "na kama nyundo ya chuma inayopasua-pasua jabali?"^c

30 "Basi nitawaadhibu manabii," asema Yehova, "wanaoibiana maneno yangu."^d

31 "Nitawaadhibu manabii," asema Yehova, "wanaotumia ulimi wao kusema, 'Anasema hivi!'"^e

32 "Nitawaadhibu manabii wa ndoto za uwongo," asema Yehova, "wanaozisimulia na kuwapotosha watu wangu kwa sababu ya uwongo wao na kujigamba kwao."^f

"Lakini sikuwatuma wala kuwaamuru. Basi hawatawafaidi watu hawa hata kidogo,"^g asema Yehova.

33 "Na watu hawa au nabii au kuhani akiwauliza, 'Mzigo* wa Yehova ni nini?' mtawajibu hivi: "'Ninyi watu ndio mzigo! Nami nitawatupa,'"^h asema Yehova.' **34** Naye nabii au kuhani au mtu anayesema, 'Huu ndio mzigo* wa Yehova!' Nitamkazia fikira mtu huyo na nyumba yake. **35** Hivi ndivyo kila mmoja wenu anavyomwambia mwenzake na pia ndugu yake, 'Yehova ametoa jibu gani? Na Yehova amese-

23:33 *Au "Ujumbe unaochosha." Neno hilo la Kiebrania lina maana mbili: "ujumbe mzito kutoka kwa Mungu" au "kitu kinachochosha." **23:34** *Au "ujumbe unaochosha."

ma nini?' **36** Lakini msitaje tena mzigo* wa Yehova, kwa maana mzigo* ni neno la kila mtu binafsi, nanyi mmeyabadili maneno ya Mungu aliye hai, Yehova wa majeshi, Mungu wetu.

37 "Utamuuliza nabii huyo hivi: 'Yehova amekupa jibu gani? Na Yehova amesema nini?' **38** Nanyi mkiendelea kusema, "Mzigo# wa Yehova!" Yehova anasema hivi: "Kwa sababu mnasema, 'Hili neno ndilo mzigo* wa Yehova,' baada ya mimi kuwaambia, 'Msi- seme: "Mzigo# wa Yehova!"' **39** tazameni! Nitawainu juu na kuwatupia kutoka mbele zangu, ninyi pamoja na jiji nililowapa ninyi na mababu zenu. **40** Nami nitawaletea aibu ya milele na fedheha ya milele, ambayo haitasahauliwa."'''^a

24 Kisha Yehova akanionyesha vikapu viwili vya tini vilivyowekwa mbele ya hekalu la Yehova, baada ya Mfalme Nebukadnezah* wa Babiloni kumpeleka uhamishoni Yekonia#^b mwana wa Yehoyakimu,^c mfalme wa Yuda, pamoja na wakuu wa Yuda, mafundi, na wahunzi;^d aliwatoa Yerusalemu na kuwapeleka Babiloni.^d **2** Kikapu kimoja kilikuwa na tini nzuri sana, kama tini za mapema, lakini kile kikapu kingine kilikuwa na tini mbaya sana, zilikuwa mbaya sana hivi kwamba hazingewezi kuliwa.

3 Kisha Yehova akaniluliza: "Unaona nini, Yereimia?" Basi

23:36, 38 *Au "ujumbe unaochosha." 23:38 #Au "Ujumbe unaochosha." 24:1 *Tnn., "Nebukadrezah," njia nyingine ya kuandika jina hili. #Pia anaitwa Yehoyakini na Konia. ^aAu labda, "wajenzi wa maboma ya ulinzi."

SURA YA 23

a Yer 24:9
Yer 42:18
Omb 5:20
Da 9:16

SURA YA 24

b Yer 22:24

c 2Fa 24:6
1Nya 3:16

d 2Fa 24:15, 16
Yer 29:1, 2

Safu ya 2

a Yer 24:8

b Ezz 1:3
Yer 12:15
Yer 25:11
Yer 29:10
Eze 36:24

c Yer 1:10
Yer 30:18
Yer 32:41

d Kum 30:6
Yer 31:33
Eze 11:19

e Yer 30:22
Yer 32:38
Zek 8:8

f Yer 29:13

g Yer 29:17

h 2Fa 25:6, 7
Eze 12:12, 13

i Yer 44:1
Yer 46:13

j Yer 15:4
Yer 34:17

k Yer 26:4, 6
Yer 29:22

l Kum 28:64
Yer 29:18

m Law 26:33
Yer 9:16

n Kum 28:59
Yer 15:2
Eze 7:15

SURA YA 25

o 2Fa 24:1
Yer 36:1
Yer 46:2
Da 1:1

nikasema: "Tini; tini nzuri ni nzuri sana, na tini mbaya ni mbaya sana, hivi kwamba haziwezi kuliwa."^a

4 Ndipo neno la Yehova likanijia likisema: **5** "Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: 'Kama hizi tini nzuri, ndivyo nitakavyowaona kwa njia nzuri wale watu wa Yuda walihamishwa, ambao nimewatoa mahali hapa na kuwapeleka katika nchi ya Wakaldayo. **6** Jicho langu litaendelea kuwatazama kwa faida yao, nami nitawarudisha katika nchi hii.^b Nitawajenga, nami sitawabomoa; nitawapanda, nami sitawang'oa.^c **7** Nami nitawapa moyo wa kunijua, kwamba mimi ni Yehova.^d Watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao,^e kwa maana watarudi kwangu kwa moyo wao wote.^f

8 "Lakini kuhusu tini mbaya ambazo ni mbaya sana hivi kwamba haziwezi kuliwa,^g Yehova anasema hivi: "Ndivyo nitakavyomwona Mfalme Sedekia^h wa Yuda, wakuu wake, wakaaji wa Yerusalemu waliobaki katika nchi hii, na wale wanaokaa nchini Misri.ⁱ **9** Nitawafanya wawe kitu cha kutisha na msiba kwa falme zote za dunia,^j shutuma, methali, kitu cha kudhihakiwa, na laana^k kila mahali nitakapowatawanya.^l **10** Nami nitawaletea upanga,^m njaa kali, na ugonjwa hatari,ⁿ mpaka waangamie kutoka katika nchi niliyowapa wao na mababu zao."^m

25 Neno lililomjia Yereimia kuhusu watu wote wa Yuda katika mwaka wa nne wa utawala wa Yehoyakimu^o mwana wa Yosia, mfalme wa

Yuda, ambao ulikuwa mwaka wa kwanza wa Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni. **2** Nabii Yerebia alisema hivi kuhusu* watu wote wa Yuda na wakaaji wote wa Yerusalemu:

3 "Tangu mwaka wa 13 wa utawala wa Yosia^a mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda, mpaka leo hii, miaka hii 23, neno la Yehova limenijia, nami niliendelea kuwaambia tena na tena,* lakini hamkusikiliza.^b **4** Na Yehova aliwatumia kwenu watumishi wake wote manabii, aliwatumia tena na tena,* lakini hamkusikiliza, wala kutega sikio lenu ili msikie.^c **5** Walikuwa wakisema, "Tafadhali, geukeni kila mmoja wenu kutoka katika njia zenu za uovu na matendo yenu maovu;^d nanyi mtaendelea kukaa kwa muda mrefu katika nchi ambayo Yehova aliwapa ninyi na mababu zenu zamani. **6** Msiifuute miungu mingine na kuiabudu na kui-namia, na kunikasirisha kwa kazi ya mikonu yenu; la sivyo nitawaletea msiba."

7 "Lakini hamkunisikiliza," asema Yehova, "Badala yake mlinikasirisha kwa kazi ya mikonu yenu, na kujiletea msiba."^e

8 "Kwa hiyo Yehova wa majeshi anasema hivi: "Kwa sababu hamkuyatii maneno yangu, **9** ninaziita familia zote za kaskazini,"^f asema Yehova, "ninamwita Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni, mtumishi wangu,^g nami nitawaletea dhidi ya nchi hii^h na dhidi ya wa-

25:1, **9** *Tnn., "Nebukadreza," njia nyingine ya kuandika jina hili. 25:2 *Au "aliwaambia hivi." 25:3 *Tnn., "kuamka mapema na kusema." 25:4 *Tnn., "akiama mapema na kuwatumia."

SURA YA 25

a Yer 1:2

b Yer 7:13
Yer 13:10

c Yer 29:19

d 2Fa 17:13
Isa 55:7
Yer 18:11
Yer 35:15
Eze 18:30
Eze 33:11e Kum 32:21
Ne 9:26f Law 26:25
Isa 5:26
Yer 1:15g Yer 27:6
Yer 43:10h Kum 28:49, 50
Yer 5:15
Eze 7:24

Safu ya 2

a Eze 26:7
Eze 29:19
Hab 1:6b Isa 24:7
Eze 26:13

c Yer 7:34

d 2Nya 36:20, 21
Da 9:2
Zek 1:12
Zek 7:5e Kum 30:3
Ezr 1:1, 2
Yer 29:10f Isa 47:1
Yer 51:1
Da 5:26, 30g Isa 13:1, 19
Isa 14:4, 23h Yer 50:9
Yer 51:27i Isa 14:2
Hab 2:8j Zb 137:8
Yer 50:29
Yer 51:6, 24
Ufu 18:6k Yer 51:7
Omb 4:21
Eze 23:32-34
Nah 3:7, 11

kaaji wake na dhidi ya mataifa haya yote yanayozunguka.^a Nitawaangamiza na kuwafanya kuwa kitu cha kutisha na kitu cha kupigiwa mluzi na magofu ya kudumu. **10** Nitakomesha sauti ya furaha na sauti ya shangwe ndani yao,^b sauti ya bwana harusi na sauti ya bibi harusi,^c sauti ya jiwe la kusagia na nuru ya taa. **11** Na nchi hii yote itakuwa magofu na kitu cha kutisha, na mataifa haya yatalazimika kumtumikia mfalme wa Babiloni kwa miaka 70."^d

12 "Lakini miaka 70 itakopotimia,^e nitamfanya mfalme wa Babiloni awajibike* na pia taifa hilo kwa sababu ya kosa lao,^f asema Yehova, "nami nitafanya nchi na Wakaldayo kuwa mahame na ukiwa dai-ma.^g **13** Nitatimiza maneno yangu yote niliyosema dhidi ya nchi hiyo, yote yaliyoandikwa katika kitabu hiki ambayo Yerebia ametabiri dhidi ya mataifa yote. **14** Kwa maana mataifa mengi na wafalme wakuu^h watawafanya kuwa watumwa,ⁱ nami nitawalipa kulingana na matendo yao na kazi ya mikonu yao wenyewe."^j

15 Kwa maana Yehova Mungu wa Israeli aliniambia hivi: "Chukua kikombe hiki cha di-va'i ya ghadhabu kutoka mkononi mwangu, nawe uyanywesho mataifa yote ambayo ninakutuma kwao. **16** Nao watakunywa na kupepesuka na kutenda kama wendawazimu kwa sababu ya upanga ninaituma miongoni mwao."^k

17 Basi nikakichukua kile kikombe kutoka mkononi mwa Yehova na kuyanywesho

25:12 *Au "nitamwadhibu mfalme wa Babiloni."

mataifa yote ambayo Yehova alinituma kwao:^a **18** kuanzia Yerusalemu na majiji ya Yuda,^b wafalme wake na wakuu wake, ili kuyafanya kuwa magofu, kitu cha kutisha, kitu cha kupigiwa mluzi na laana,^c kama ilivyo leo; **19** kisha mfalme Farao wa Misri na watumishi wake, wakuu wake, na watu wake wote,^d **20** na watu wa mataifa mbalimbali waliochanganama nao; wafalme wote wa nchi ya Usi; wafalme wote wa nchi ya Wafilisti,^e Ashkeloni,^f Gaza, Ekroni, na watu waliobaki wa Ashdodi; **21** Edo mu,^g Moabu,^h na Waamoni;ⁱ **22** wafalme wote wa Tiro, wafalme wote wa Sidoni,^j na wafalme wa kisiwa kilicho baharini; **23** Dedani,^k Tema, Buzi, na wale wote wanaonyoa nywele pembeni mwa vichwa vyao;^l **24** wafalme wote wa Waarabu^m na wafalme wote wa watu wa mataifa mbalimbali wanaokaa nyikani; **25** wafalme wote wa Zimri, wafalme wote wa Elamu,ⁿ na wafalme wote wa Wamedi;^o **26** na wafalme wote wa kaskazini walio karibu na walio mbali, mmoja baada ya mwingine, na falme nyingine zote za dunia zilizo juu ya ardhi; na mfalme wa Sheshaki*^p atakunywa baada yao.

27 "Nawe unapaswa kuwaambia, 'Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: "Kunyweni, mleme, mtapike na kuanguka hivi kwamba msiweze kusimama^q kwa sababu ya upanga ninaotuma miongoni mweenu."^r **28** Nao wakikataa kuki-

25:26 *Inaonekana hili ni jina la siri la Babeli (Babiloni).

SURA YA 25

a Yer 1:10

b Isa 51:17

c Yer 24:9

d Yer 46:2

e Yer 47:1

f Yer 47:5

g Yer 49:17
Omb 4:21

h Yer 48:1

i Yer 49:1

j Yer 27:2, 3
Yer 47:4

k Yer 49:8

l Yer 9:25, 26
Yer 49:32

m Yer 49:31, 32

n Yer 49:34

o Yer 51:11

p Yer 51:41

q Isa 63:6
Hab 2:16

Safu ya 2

a 1Fa 9:7
Yer 7:12, 14
Da 9:18
Ho 12:2
Mik 6:2b Yer 49:12
Oba 16

c Yoe 3:2

d Isa 34:2, 3
Yer 25:17

chukua kikombe kutoka mkononi mwako ili wanywe, waa mbie, 'Yehova wa majeshi anasema hivi: "Lazima mnywe! **29** Kwa maana tazama! ikiwa ninaleta msiba kwanza juu ya jiji linaloitwa kwa jina langu,^a je, ninyi pia hampaswi kuadhibiwa?"^b

"Hamtakosa kuadhibiwa, kwa maana ninaita upanga dhidi ya wakaaji wote wa dunia,' asema Yehova wa majeshi.

30 "Nawe unapaswa kuwatabiria maneno haya yote, uwaambie,

'Yehova atanguruma kutoka juu,

Kutoka katika makao yake matakatifu atafanya sauti yake isikike.

Atanguruma kwa sauti kubwa dhidi ya makao yake yanayodumu.

Atapaza sauti kama watu wanaokanyaga shinikizo la divai,

Ataimba kwa ushindi dhidi ya wakaaji wote wa dunia.'

31 'Kelele zitasikika mpaka kwenye miisho ya dunia, Kwa maana Yehova ana kesi dhidi ya mataifa. Yeye binafsi atawahukumu wanadamu wote.*^c

Naye atawaangamiza wavu kwa upanga,' asema Yehova.

32 Yehova wa majeshi anasema hivi:

'Tazameni! Msiba unaenea kutoka taifa mpaka taifa,^d

25:31 *Tnn., "wote wenye mwili wa nyama."

Na tufani kubwa itaachi-liwa kutoka sehemu za mbali zaidi za dunia.^a

33 “Na wale ambao Yehova atawaua siku hiyo watata-pakaa kutoka mwisho mmo-ja wa dunia mpaka mwisho wa pili wa dunia. Hawataombole-zewa, wala kukusanywa wala kuzikwa. Watakuwa kama mbolea juu ya ardhi.”

34 “Ombolezeni, enyi wachu-ngaji, na mlie kwa sauti! Mgaegae, enyi watu ma-shuhuri wa kundi, Kwa sababu wakati wenu wa kuchinjwa na kutawa-nywa umefika, Nanyi mtaanguka kama chombo chenye tha-mani!

35 Wachungaji hawana ma-hali pa kukimbilia, Na watu mashuhuri wa kundi hawawezi kupo-nyoka.

36 Sikilizeni! Kilio cha wa-chungaji Na kuomboleza kwa watu mashuhuri wa kundi, Kwa maana Yehova anaha-ribu malisho yao.

37 Na makao yenye amani yamefanywa yasiwe na uhai Kwa sababu ya hasira ya Yehova inayowaka.

38 Ametoka katika pango lake kama mwana-simba,^{*b} Kwa maana nchi yao ime-kuwa kitu cha kutisha Kwa sababu ya upanga we-nye ukatili Na kwa sababu ya hasira yake inayowaka.”

25:38 *Au “mwanasimba mwenye ma-nyoya marefu shingoni.”

SURA YA 25

a Sef 3:8

b Ho 5:14

Safu ya 2

SURA YA 26

a 2Fa 23:34
2Nya 36:4
Yer 25:1
Yer 35:1
Yer 36:1b Isa 55:7
Yer 18:7, 8
Yer 36:3
Eze 18:27c 2Fa 17:13, 14
Yer 7:12-14
Yer 25:3

d Zb 78:60

e Yer 24:9

f Yer 26:2

26 Mwanzoni mwa utawala wa Yehoyakimu^a mwa-na wa Yosia, mfalme wa Yuda, neno hili lilikuja kutoka kwa Yehova: **2** “Yehova anasema hivi: ‘Simama katika ua wa nyumba ya Yehova useme kuhusu* watu wote wa maji-ji ya Yuda wanaoingia ili kua-budu[#] katika nyumba ya Yehova. Waambie kila kitu ni-nachokuamuru; usiondoe hata neno moja. **3** Labda watasi-kiliza na kila mmoja ataiacha njia yake ovu, nami nitaba-dili nia yangu* kuhusu msi-ba ninaokusudia kuwaletea kwa sababu ya matendo yao maovu.^b **4** Waambie, “Yehova anasema hivi: ‘Ikiwa ha-mtanisikiliza kwa kufuata she-ria* yangu niliyoweka mbe-le yenu, **5** kwa kuyasikiliza maneno ya watumishi wangu manabii, ninaowatuma kwenu tena na tena,* ambao hamja-wasikiliza,^c **6** basi nitaifanya nyumba hii kama Shilo,^d nami nitalifanya jiji hili kuwa kitu cha kulaaniwa na mataifa yote ya dunia.’”^e

7 Na makuhani na manabii na watu wote wakamsikia Ye-remia akisema maneno hayo ndani ya nyumba ya Yehova.^f **8** Yeremia alipomaliza kuse-ma mambo yote ambayo Yehova alimwamuru awaambie watu wote, ndipo makuhani na manabii na watu wote waka-mkamata na kusema: “Hakika utakufa. **9** Kwa nini umetabi-ri katika jina la Yehova, ukise-ma, ‘Nyumba hii itakuwa kama Shilo, na jiji hili litaangami-zwa na kuachwa bila mkaaji?’”

26:2 *Au “uwaambie.” #Au “kuinama.”
26:3 *Au “nitaghairi.” 26:4 *Au “ma-fundisho.” 26:5 *Tnn., “ambao ninaa-mka mapema na kuwatuma.”

Na watu wote wakakusanyika kumzunguka Yeremia ndani ya nyumba ya Yehova.

10 Wakuu wa Yuda waliposikia maneno hayo, wakapanda kutoka katika nyumba ya* mfalme wakawaenda katika nyumba ya Yehova na kuketi kwenye njia inayoelekea kwenye lango jipya la Yehova.^a **11** Makuhani na manabii wakawaambia hivi wakuu na watu wote: “Mtu huyu anastahili hukumu ya kifo,^b kwa sababu ametabiri dhidi ya jiji hili kama mlivyosikia kwa masikio yenu wenyewe.”^c

12 Ndipo Yeremia akawaambia wakuu wote na watu wote: “Yehova ndiye aliyenituma kutabiri dhidi ya nyumba hii na dhidi ya jiji hili maneno yote ambayo mmeyasikia.”^d

13 Basi sasa rekebisha njia zenu na matendo yenu nanyi mtii sauti ya Yehova Mungu wenu, naye Yehova atabadili nia yake* kuhusu msiba aliotangaza dhidi yenu.^e **14** Lakini mimi niko mikononi mwenu. Nitendeeni jambo lote mnalooa kuwa jema na sawa machoni penu. **15** Ila tu mjue kwa hakika kwamba mkiniua, mtajiletea damu isiyoyana hatia juu yenu na juu ya jiji hili na juu ya wakaaji wake, kwa maana kwa kweli Yehova alinituma kwenu ili niseme maneno haya mkiyasikia.”

16 Ndipo wakuu na watu wote wakawaambia makuhani na manabii: “Mtu huyu hastahili hukumu ya kifo, kwa maana alizungumza nasi katika jina la Yehova Mungu wetu.”

17 Zaidi ya hayo, baadhi ya wazee wa nchi wakasimama

26:10 *Au “jumba la.” **26:13** *Au “ataghairi.”

SURA YA 26

a Yer 36:10

b Yer 18:19, 20

c Yer 38:4

d Yer 1:17

e Yer 7:3
Yer 36:3
Eze 18:32
Yon 3:9

Safu ya 2

a Mik 1:1

b 2Nya 29:1

c Zb 79:1
Yer 9:11

d Mik 3:12

e 2Nya 32:26

f Yos 15:20, 60
Yos 18:11, 14
1Sa 7:2

g 2Fa 23:34
2Nya 36:5

h 2Nya 16:10

i Yer 36:11, 12

na kuanza kuliambia hivi kutaniko lote la watu: **18** “Mika^a wa Moreshethi alikuwa akitabiri katika siku za utawala wa Mfalme Hezekia^b wa Yuda, akawaambia watu wote wa Yuda, ‘Yehova wa majeshi anasema hivi:

“Sayuni litalimwa kama shamba,

Yerusalemu litakuwa marundo ya magofu,^c

Na mlima wa Nyumba* utakuwa kama vilima msituni.”^{#d}

19 “Je, Mfalme Hezekia wa Yuda na watu wote wa Yuda walimuua? Je, hakumwogopa Yehova na kumwomba Yehova kibali,* hivi kwamba Yehova akabadili nia yake[#] kuhusu msiba aliotangaza dhidi yao?^e Basi tuko karibu kujiletea msiba mkubwa.

20 “Na kulikuwa na mtu mwingine aliyetabiri katika jina la Yehova, Uriya mwana wa Shemaya kutoka Kiriath-yearimu,^f aliyetabiri dhidi ya jiji hili na dhidi ya nchi hii kwa maneno kama ya Yeremia. **21** Mfalme Yehoyakimu^g na wanaume wake wote hodari na wakuu wote wakayasikia maneno yake, na mfalme alitaka kumuua.^h Uriya aliposikia jambo hilo, mara moja akaogopa na kukimbilia Misri. **22** Kisha Mfalme Yehoyakimu akamtuma Elnathaniⁱ mwana wa Akbori pamoja na watu wengine kwenda Misri. **23** Wakamchukua Uriya kutoka Misri na kumpeleka kwa Mfalme Yehoyakimu,

26:18 *Au “mlima wa hekalu.” #Au “kilima chenye msitu.” **26:19** *Au “hakujaribu kuutuliza uso wa Yehova.” #Au “akaghairi.”

naye akamuua kwa upanga^a na kuitupa maiti yake katika makaburi ya watu wa kawaida.”

24 Lakini Ahikamu^b mwana wa Shafani^c alimsaidia Yere-mia, ili asitiwe mikononi mwa watu na kuuawa.^d

27 Mwanzoni mwa utawala wa Yehoyakimu mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, neno hili lilimjia Yere-mia kutoka kwa Yehova: **2** “Yehova ameniambia hivi: ‘Jitenge-neeze mikanda na nira, nawe uziweke kwenye shingo yako. **3** Kisha upeleke vitu hivyo kwa mfalme wa Edomu,^e mfalme wa Moabu,^f mfalme wa Waamoni,^g mfalme wa Tiro,^h na kwa mfalme wa Sidoniⁱ kwa mkono wa wajumbe waliokuja Yerusalemu kwa Mfalme Sedekia wa Yuda. **4** Uwape amri hii kwa ajili ya mabwana wao:

““Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema; waambieni hivi mabwana wenu: **5** ‘Mimi ndiye niliyeiumba dunia, wanadamu, na wanyama walio duniani kwa nguvu zangu kuu na kwa mkono wangu ulionyoo-shwa; nami nimempa yeyote ninayetaka.*^j **6** Na sasa mimi mwenyewe nimezitia nchi hizi zote mikononi mwa mtumishi wangu Mfalme Nebukadneza^k wa Babiloni; nimempa hata wanyama wa mwituni ili wamtumikie. **7** Mataifa yote yatatumikia yeye na mwanawe na mjukuu wake mpaka wakati wa nchi yake utakapofika,^l wakati ambapo mataifa mengi na wafalme wakuu watamfanya kuwa mtumwa wao.’^m

27:5 *Tnn., “yule anayefaa machoni pangu.”

SURA YA 26

a Yer 2:30

b 2Fa 22:12, 13
Yer 39:13, 14
Yer 40:5

c 2Fa 22:10

d 1Fa 18:4

SURA YA 27

e Eze 25:12, 13
Oba 1

f Yer 48:1
Eze 25:8, 9

g Yer 49:1, 2
Eze 25:2

h Isa 23:1
Yer 47:4
Eze 26:3

i Isa 23:4
Eze 28:21
Yoe 3:4

j Da 4:17

k Yer 25:9
Yer 28:14
Yer 43:10
Da 2:37, 38

l Zb 137:8
Yer 50:14, 27
Da 5:26, 30

m Yer 25:12, 14
Yer 51:11

Safu ya 2

a Eze 26:7, 8

b 2Fa 24:17
1Nya 3:15
Yer 37:1

c Yer 38:2, 20

d 2Fa 25:7

e 2Fa 25:3

f Yer 21:9
Eze 14:21

g Yer 28:1, 2
Yer 28:11
Yer 37:19

h Yer 14:14
Yer 23:21

Yer 28:15
Yer 29:8, 9
Eze 13:6

8 ““““Tkiwa taifa lolote au ufalme utakataa kumtumikia Mfalme Nebukadneza wa Babiloni na kukataa kuweka shingo yake chini ya nira ya mfalme wa Babiloni, nitalia-dhibu taifa hilo kwa upanga,^a kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari,’ asema Yehova, ‘mpaka nitakapowaangamiza kwa mkono wake.’

9 ““““Kwa hiyo, msiwasikilize manabii wenu, waaguzi* wenu, waota-ndoto wenu, wachawi wenu, na walozi wenu, wanaowaambia: “Hamtamtumikia mfalme wa Babiloni.” **10** Kwa maana wanawatabiria uwongo, ili mpeleke mballi na nchi yenu, nami nitawatawanya ninyi, nanyi mtaangamia.

11 ““““Lakini taifa litakaloweke shingo yake chini ya nira ya mfalme wa Babiloni na kumtumikia, nitaliruhusu libaki* kwenye nchi yake,’ asema Yehova, ‘ili kuilima na kukaa ndani yake.’”””

12 Pia nilimwambia Mfalme Sedekia^b wa Yuda maneno hayohayo, nikisema: “Weken shingo zenu chini ya nira ya mfalme wa Babiloni na mmtumikie yeye na watu wake, nanyi mtaendelea kuishi.^c **13** Kwa nini wewe na watu wako mfe kwa upanga,^d kwa njaa kali,^e na kwa ugonjwa hatari,^f kama Yehova alivyosema kuhusu taifa ambalo halitamtumikia mfalme wa Babiloni? **14** Msiyasikilize maneno ya manabii wanaowaambia, ‘Hamtamtumikia mfalme wa Babiloni,’^g kwa sababu wanawatabiria uwongo.^h

27:9 *Au “wabashiri.” **27:11** *Tnn., “lipumzike.”

15 “Kwa maana sijawatuma,’ asema Yehova, ‘lakini watabiri uwongo katika jina langu, ili mwishowe niwatawanye na mwangamie, ninyi na manabii wanaowatabiria ninyi.”^a

16 Nami nikawaambia makuhani na watu hawa wote, “Yehova anasema hivi: ‘Msiyasikilize maneno ya manabii wenu wanaowatabiria wakisema: “Tazameni! Vyombo vya nyumba ya Yehova vitarudishwa kutoka Babiloni hivi karibuni!”^b kwa maana wanawatabiria uwongo.^c 17 Msiwasikilize. Mtumikieni mfalme wa Babiloni nanyi mtaendelea kuishi.^d Kwa nini jiji hili liwe magofu? 18 Lakini ikiwa wao ni manabii na ikiwa wana neno la Yehova, tafadhali acheni wamwombe Yehova wa majeshi kwamba vyombo vilivyobaki katika nyumba ya Yehova, katika nyumba ya* mfalme wa Yuda, na Yerusalemu visipelekwe Babiloni.’

19 “Kwa maana Yehova wa majeshi anasema hivi kuhusu zile nguzo,^e ile Bahari,^f yale magari,^g na vyombo vilivyobaki vilivyoachwa katika jiji hili, 20 ambavyo Mfalme Nebukadneza wa Babiloni hakuvichukua alipompeleka uhamishoni Yekonia mwana wa Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, kutoka Yerusalemu hadi Babiloni, pamoja na watu wote wenyewe vyeo wa Yuda na Yerusalemu;^h 21 naam, Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli anasema hivi kuhusu vyombo vilivyobaki katika nyumba ya Yehova, katika nyumba ya*

27:18, 21 *Au “jumba la.” 27:19 *Yaa-ni, Bahari ya shaba ya hekalu.

SURA YA 27

a Yer 20:6
Yer 29:21
Eze 13:3

b 2Fa 24:11, 13
2Nya 36:7
Yer 28:1-3
Da 1:1, 2

c Yer 14:13

d Yer 27:11
Yer 38:17

e 1Fa 7:15
2Fa 25:17
2Nya 4:11, 12
Yer 52:21

f 1Fa 7:23

g 1Fa 7:27
2Fa 25:16
2Nya 4:11, 14

h 2Fa 24:14, 15
2Nya 36:10
Yer 24:1
Da 1:2, 3

Safu ya 2

a 2Fa 25:13, 14
2Nya 36:18
Yer 52:17, 18
Da 5:3

b Ezz 1:7
Ezz 5:14

SURA YA 28

c 2Fa 24:17
2Nya 36:10

d Yos 11:19
2Sa 21:2

e Yer 27:4, 8

f 2Fa 24:11, 13
Yer 27:16
Da 1:2

g 2Fa 24:8
2Fa 25:27
Yer 37:1

h 2Fa 23:36
2Fa 24:6

i 2Fa 24:12, 14
Yer 24:1

mfalme wa Yuda, na Yerusalemu: 22 “Vitapelekwa Babiloni,^a navyo vitabaki huko mpaka siku nitakapovikazia fikira,” asema Yehova. “Kisha nitavileta na kuvirudisha mahali hapa.”^b

28 Mwaka huohuo, mwanzoni mwa utawala wa Mfalme Sedekia^c wa Yuda, katika mwaka wa nne, mwezi wa tano, nabii Hanania mwana wa Azuri kutoka Gibeoni^d aliniambia hivi katika nyumba ya Yehova mbele ya makuhani na watu wote: 2 “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi, ‘Nitai-vunja nira ya mfalme wa Babiloni.^e 3 Katika muda wa miaka miwili* nitavirudisha mahali hapa vyombo vyote vya nyumba ya Yehova ambavyo Mfalme Nebukadneza wa Babiloni alivichukua mahali hapa na kuvipeleka Babiloni.’^f 4 “Nami nitamrudisha mahali hapa Yekonia^g mwana wa Yehoyakimu,^h mfalme wa Yuda, na watu wote wa Yuda waliohamishwa na kuvipelekwa Babiloni,ⁱ asema Yehova, ‘kwa maana nitaivunja nira ya mfalme wa Babiloni.’”

5 Kisha nabii Yeremia akazungumza na nabii Hanania mbele ya makuhani na watu wote waliokuwa wamesimama katika nyumba ya Yehova. 6 Nabii Yeremia akasema: “Amina!* Yehova na afanye hivyo! Yehova na atimize maneno yako uliyotabiri kwa kuvirudisha mahali hapa vyombo vya nyumba ya Yehova kutoka Babiloni na pia watu wote waliopelekwa uhamishoni!

28:3 *Tnn., “miaka miwili ya siku.” 28:6 *Au “Na iwe hivyo!”

7 Hata hivyo, tafadhali sikia ujumbe huu ninaosema masikioni mwako na masikioni mwa watu wote. 8 Zamani za kale manabii walionitangulia mimi na waliokutangulia wewe walikuwa wakitabiri kuhusu nchi nyingi na falme kubwa, kuhusu vita, misiba, na magonjwa hatari. 9 Nabii akitabiri amani na neno la nabii huyo litimie, basi itajulikana kwamba kwa kweli Yehova amemtuma nabii huyo.”

10 Ndipo nabii Hanania akaichukua ile nira kutoka shingoni mwa nabii Yeremia na kuivunja.^a 11 Kisha Hanania akasema mbele ya watu wote: “Yehova anasema hivi: ‘Hivyo ndivyo nitakavyoivunja nira ya Mfalme Nebukadneza wa Babiloni kutoka shingoni mwa mataifa yote katika muda wa miaka miwili.’”^b Kisha nabii Yeremia akaenda zake.

12 Baada ya nabii Hanania kuivunja ile nira kutoka shingoni mwa nabii Yeremia, ujumbe huu wa Yehova ukamjia Yeremia: 13 “Nenda umwambie Hanania, ‘Yehova anasema hivi: “Umevunja nira za mbao,^c lakini badala yake utatengeneza nira za chuma.” 14 Kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Nitaweka nira ya chuma juu ya shingo ya mataifa haya yote, ili yamtumikie Mfalme Nebukadneza wa Babiloni, nayo lazima yamtumikie.^d Nitampa hata wanyama wa mwituni.””^e

15 Kisha nabii Yeremia akamwambia nabii Hanania: “Tafadhali, sikiliza, ewe Hanania! Yehova hakukutuma

SURA YA 28

a Yer 27:2

b Yer 28:4

c Yer 27:2

d Kum 28:48
Yer 5:19e Yer 27:6
Da 2:37, 38

f Yer 28:1

Safu ya 2

a Yer 14:14
Yer 23:21
Yer 27:15
Eze 13:3b Kum 13:5
Kum 18:20
Yer 29:32

SURA YA 29

c 2Fa 24:8
Yer 22:24

d Yer 22:26

e 2Fa 24:15, 16
Yer 24:1f 2Fa 22:8
Yer 26:24
Yer 39:13, 14
Eze 8:11

g 2Fa 24:18

wewe, bali umewafanya watu hawa wautumaini uwongo.^a

16 Kwa hiyo Yehova anasema hivi: “Tazama! Ninakuondoa katika uso wa nchi. Utakufa mwaka huu, kwa maana ume-wachochea watu wamwasi Yehova.”^b

17 Basi nabii Hanania akafa mwaka huo, katika mwezi wa saba.

29 Haya ndiyo maneno ya barua ambayo nabii Yeremia aliwatumia kutoka Yerusalemu wazee waliobaki miongoni mwa watu waliopelekwa uhamishoni, makuhani, manabii, na watu wote, ambao Nebukadneza alikuwa amewatoa Yerusalemu na kuwapeleka uhamishoni Babiloni, 2 baada ya Mfalme Yekonia^c na mama malkia,^d maofisa wa makao ya mfalme, wakuu wa Yuda na Yerusalemu, na mafundi na wahunzi* kuondoka Yerusalemu.^e 3 Aliituma barua hiyo kwa mkono wa Elasa mwana wa Shafani^f na Gemaria mwana wa Hilikia, ambao Mfalme Sedekia^g wa Yuda aliwatuma kwenda Babiloni kwa Mfalme Nebukadneza wa Babiloni. Barua hiyo ilisema hivi:

4 “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anawaambia hivi watu wote waliohamishwa, ambao aliwafanya wapolekwe uhamishoni Babiloni kutoka Yerusalemu, 5 ‘Jengeni nyumba mkae ndani yake. Pandeni bustani na mle matunda yake. 6 Oeni wake mzae wana na mabinti; wachukulieni wana wenu wake na kuwaoza mabinti wenu, ili wao pia wazae wana na mabi-

29:2 * Au labda, “wajenzi wa maboma ya ulinzi.”

nti. Muwe wengi huko, msipungue. **7** Nanyi tafuteni amani kwa ajili ya jiji ambamo ni-mewapeleka uhamishoni, nanyi msali kwa Yehova kwa ajili ya jiji hilo, kwa maana jiji hilo likiwa na amani mtakuwa na amani.^a **8** Kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Msiwaruhusu manabii wenu na waaguzi* wenu walio miongoni mweni wawadanganye,^b nanyi msisikilize ndoto wana-zoota. **9** Kwa maana ‘wana-watabiria uwongo katika jina langu. Mimi sijawatuma,’^c asema Yehova.””

10 “Kwa maana Yehova anasema hivi: ‘Miaka 70 itakapotimia huko Babiloni nitawakazia ninyi fikira,^d nami nitatimiza ahadi yangu kwa kuwaridisha mahali hapo.’^e

11 “Kwa maana ninajua vizuri mawazo ninayofikiria kuwaelekea ninyi,’ asema Yehova, ‘mawazo ya amani, wala si ya msiba,^f ili niwape ninyi wakati ujao na tumaini.^g **12** Nanyi mtaniita na kuja na kusali kwangu, nami nitawasikiliza.’^h

13 “Mtanitafuta na kuni-pata,ⁱ kwa maana mtanitafuta kwa moyo wenu wote.^j **14** Nami nitawaruhusu mni-pate,^k asema Yehova. ‘Nami nitawakusanya mateka wenu na kuwakusanya ninyi pamoja kutoka katika mataifa yote na sehemu zote nilizowatawanya,’^l asema Yehova. ‘Nami nitawarudisha mahali nilipowatoa nikawapeleka uhamishoni.’^m

15 “Lakini ninyi mmesema, ‘Yehova ametuinulia manabii katika Babiloni.’

29:8 *Au “wabashiri.”

SURA YA 29

a 1Ti 2:1, 2

b Yer 14:14
Yer 27:14

c Yer 23:21
Yer 28:15

d 2Nya 36:20, 21
Ezr 1:1-3
Da 9:2
Zek 1:12

e Kum 30:3
Ezr 2:1
Yer 24:6

f Sef 3:15

g Yer 31:17

h Da 9:3

i Law 26:40

j Kum 4:29
Kum 30:1-4
1Fa 8:47, 48
Yer 24:7

k Isa 55:6

l Isa 49:25
Yer 30:3
Eze 39:28

m Zb 126:1
Ho 6:11
Amo 9:14
Sef 3:20

Safu ya 2

a Yer 28:1

b Yer 24:10

c Yer 24:2, 8

d Law 26:33

e Kum 28:25
Yer 34:17

f 1Fa 9:8
2Nya 29:8
Yer 25:9
Omb 2:15

g Yer 24:9

h Yer 7:13

i Yer 6:19

j Yer 14:14
Yer 29:8
Omb 2:14

16 “Kwa maana Yehova anamwambia hivi mfalme anayeketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi^a na watu wote wanaokaa katika jiji hili, ndugu zenu ambao hawakwenda pamoja nanyi uhamishoni, **17** ‘Yehova wa majeshi anasema hivi: “Tazameni, ninatuma dhidi yao upanga, njaa kali, na ugonjwa hatari,^b nami nitawafanya kuwa kama tini zilizoza* ambazo ni mbaya sana hivi kwamba haziwezi kuliwa.””^c

18 “Nami nitawafuatia kwa upanga,^d kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari, nami nitawafanya wawe kitu cha kutisha kwa falme zote za dunia,^e na laana, na kitu cha kushangaza, kitu cha kupigiwa mluzi,^f na shutuma miongoni mwa mataifa yote ambako nitawatawanya,^g **19** kwa sababu hawakuyasikiliza maneno yangu niliyowapa kupitia watumishi wangu manabii,’ asema Yehova, ‘ambao niliwatuma tena na tena.’”^h

“Lakini hamkusikiliza,ⁱ asema Yehova.

20 “Kwa hiyo, sikieni neno la Yehova, ninyi nyote mliopeleka uhamishoni, niliowatoa Yerusalem na kuwapeleka Babiloni. **21** Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi kuhusu Ahabu mwana wa Kolaya na kuhusu Sedekia mwana wa Maaseya, wanaowatabiria uwongo katika jina langu:’ ‘Nitawatia mikononi mwa Mfalme Nebukad-neza* wa Babiloni, naye atawaua mbele ya macho yenu.

29:17 *Au labda, “zilizopasuka.” 29:19 *Tnn., “nikiamka mapema na kuwatumama.” 29:21 *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

22 Na kile kitakachowapata kitakuwa laana itakayosemwa na watu wote wa Yuda walio uhamishoni Babiloni: “Yehova na akutendee kama Sedekia na kama Ahabu, ambao mfulame wa Babiloni aliwateketeza motoni!” **23** kwa maana wametenda kwa aibu katika Israeli,^a wakifanya uzinzi na wake za majirani wao na kusema maneno ya uwongo katika jina langu, maneno ambayo si kuwaamuru.^b

““Mimi Ndiye ninayejua, nami ni shahidi,”^c asema Yehova.”

24 “Nawe utamwambia hivi Shemaya^d wa Nehelamu: **25** ‘Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Kwa sababu ulituma barua katika jina lako kwa watu wote walio Yerusalemu, kwa Sefania^e mwana wa Maaseya, kuhani, na kwa makuhani wote, ukisema, **26** ‘Yehova amekuweka kuwa kuhani badala ya kuhani Yehoyada, ili uwe mwanngalizi wa nyumba ya Yehova, uwe msimamizi wa mwendawazimu yeyote anayetenda kama nabii na kumweka katika mikatale na katika kongwa;”^f **27** basi, kwa nini hujamkemea Yeremia wa Anathothi,^g anayetenda kama nabii wenu?^h **28** Kwa maana hata alitutumia ujumbe Babiloni, akisema: “Muda mrefu utapita! Jenjeni nyumba na mkae ndani yake. Pandeni bustani na mle matunda yake,ⁱ—”””””

29 Kuhani Sefania^j alipoisoma barua hiyo mbele ya nabii Yeremia, **30** Neno la Yehova likamjia Yeremia likisema: **31** “Watumie ujumbe watu

29:26 *Au “vyuma vya shingoni.”

SURA YA 29

a Yer 23:14

b Yer 7:9, 10
Yer 27:15c Yer 16:17
Yer 23:24

d Yer 29:31, 32

e 2Fa 25:18, 21
Yer 21:1, 2
Yer 37:3
Yer 52:24, 27

f Yer 20:2

g Yer 1:1

h Yer 43:2

i Yer 29:5

j 2Fa 25:18, 21

Safu ya 2

a Yer 14:14
Yer 28:15, 16
Eze 13:8, 9

SURA YA 30

b Kum 30:3
Eze 39:25c Eze 2:1
Yer 29:14
Yer 32:44
Eze 20:42
Amo 9:14

wote waliopelekwa uhamishoni, ukisema, ‘Yehova anasema hivi kumhusu Shemaya wa Nehelamu: “Kwa sababu Shemaya aliwatabiria, ingawa siku mtuma, naye akajaribu kuwafanya mtumaini uwongo,”^a **32** kwa hiyo Yehova anasema hivi: ‘Ninamkazia fikira Shemaya wa Nehelamu na wazao wake. Hakuna yeyote miongoni mwa watu wake atakayeokoka kati ya watu hawa, naye hataona mema nitakayowatendea watu wangu,’ asema Yehova, ‘kwa maana amewachochea watu wamwasi Yehova.’”””

30 Neno hili lilimjia Yeremia kutoka kwa Yehova, likisema: **2** “Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Andika katika kitabu maneno yote ninayokuambia. **3** Kwa maana “tazama! siku zinakuja,” asema Yehova, “nitakapowakusanya watu wangu walio tekwa, Israeli na Yuda,”^b asema Yehova, “nami nitawarudisha katika nchi niliyowapa mababu zao, nao wataimiliki tena.”””^c

4 Haya ndiyo maneno ambayo Yehova aliwaambia watu wa Israeli na Yuda.

5 Yehova anasema hivi: “Tumesikia sauti za kute-temeka;

Kuna hofu, na hakuna amani.

6 Ulizeni, tafadhali, ikiwa mwanamume anaweza kujifungua mtoto.

Hivyo basi, kwa nini ninamwona kila mwanamume mwenye nguvu akishika tumbo lake*^c

30:6 *Au “kiuno chake.”

Kama mwanamke anayeji-fungua?^a

Kwa nini kila uso umegeu-ka rangi?

- 7** Ole wangu! Kwa maana siku hiyo inatisha sana.*^b

Hakuna nyingine kama hiyo,

Wakali wa taabu kwa Yakobo.

Lakini ataokolewa kutoka-na nayo."

8 "Na siku hiyo," asema Yehova wa majeshi, "nitaivunja nira kutoka shingoni mwako, na mikanda yako nitaikata* vipande viwili; na wageni[#] hawatamfanya[^] tena kuwa mtumwa wao. **9** Watamtumikia Yehova Mungu wao na Daudi mfalme wao, ambaye nitamweka juu yao."^c

- 10** "Nawe, mtumishi wangu Yakobo, usiogope," asema Yehova, "Wala usihofu, Ee Israeli.^d Kwa maana nitakuokoa kutoka mbali Na uzao wako kutoka katika nchi waliyopelekwa utekwani.^e

Yakobo atarudi na kuwa na utulivu bila usumbufu,

Na hakuna yeyote atakayewaogopesha."^f

- 11** "Kwa maana mimi niko pamoja nawe," asema Yehova, "ili nikuokoe. Lakini nitaleta maangamizi katika mataifa yote ambako nilikutawanya;^g

30:7 *Tnn., "ni kuu." **30:8** *Tnn., "pingu zako nitazikata." [#]Au "wageni kutoka nchi nyingine." [^]Au "hawatawafanya."

SURA YA 30

a Yer 4:31
Mik 4:9

b Yoe 2:11
Sef 1:14

c Eze 34:23
Eze 37:24
Ho 3:5

d Isa 41:13

e Isa 49:25
Yer 3:18

f Yer 33:16
Eze 34:25
Ho 2:18
Mik 4:4

g Yer 50:29
Yer 51:24

Safu ya 2

a Law 26:44
Ne 9:31
Omb 3:22
Amo 9:8

b Kut 34:6, 7
Yer 46:27, 28

c 2Nya 36:15, 16
Isa 6:10
Yer 8:21, 22

d Omb 1:2, 19

e Omb 2:5

f Yer 5:6

g 2Nya 36:14

h Isa 41:11
Yer 25:12

i Yer 51:29, 56
Mik 5:9

Lakini wewe, sitakuangamiza.^a

Nitakutia nidhamu* kwa kiwango kinachofaa, Nami sitakuacha kamwe bila kukuadhibu."^b

- 12** Kwa maana Yehova anase-ma hivi:

"Hakuna matibabu kwa ajili ya jeraha lako."^c

Kidonda chako hakiwezi kupona.

- 13** Hakuna mtu wa kuku-tetea, Hakuna njia ya kukiponya kidonda chako. Hakuna dawa ya kukuponya.

- 14** Wapenzi wako wote wamekusahau.^d

Hawakutafuti tena.

Kwa maana nimekupiga kwa pigo la adui.^e

Kwa adhabu ya mtu mkatili,

Kwa sababu ya hatia yako kubwa na dhambi zako nyingi.^f

- 15** Kwa nini unapaza kilio kwa sababu ya jeraha lako?*

Maumivu yako hayawezi kupona!

Kwa sababu ya hatia yako kubwa na dhambi zako nyingi^g

Nimekutendea hivyo.

- 16** Kwa hiyo wale wote wanaokumeza, watamezwa,^h Na maadui wako wote watapelekwa pia utekwani.ⁱ Wale wanaokupora wataporwa, Nami nitawatia mikononi

30:11 *Au "Nitakurekebisha." **30:12**, **15** *Au "jeraha lako la kuvunjika."

mwa waporaji wale wote wanaokupora.”^a

- 17** “Lakini nitakurudishia afya yako na kuyaponya majeraha yako,”^b asema Yehova,
“Ingawa walikuita mtu aliyetengwa:
‘Sayuni, asiyetafutwa na yeyote.’”^c

- 18** Yehova anasema hivi:
“Ninawakusanya mateka wa mahema ya Yakobo,”^d
Nami nitayahurumia makao yake.
Jiji litajengwa upya juu ya kilima chake,^e
Na mnara wenye ngome utasimama mahali pake panapofaa.

- 19** Na kutoka kwao kutakuwa na shukrani na sauti za kicheko.^f
Nitawazidisha, nao hawatakuwa wachache;^g
Nitawafanya kuwa wengi,*
Nao hawatakuwa duni.^h

- 20** Wanawe watakuwa kama walivyokuwa zamani,
Na kusanyiko lake litaimarishwa kabisa mbele zangu.ⁱ
Nitakabiliana na wote wa-naomkandamiza.^j

- 21** Mtu wake mashuhuri atatokata kati yake,
Na mtawala wake atatoka kati yake.
Nitamfanya akaribie, naye atanikaribia.”
“La sivyo, ni nani anayeweza kuthubutu kunikaribia?”* asema Yehova.

30:19 *Au labda, “waheshimiwe.”
30:21 *Tnn., “kutoa moyo wake kuwa rehani ili anikaribie?”

SURA YA 30

a Zek 2:8, 9

b Zb 102:13
Yer 33:6, 7

c Omb 2:15

d Zb 85:1
Yer 24:6
Yer 29:10

e Mik 4:8

f Ezz 3:12
Ne 8:17
Isa 35:10

g Kum 30:5
Isa 27:6
Zek 10:8

h Isa 60:22
Mik 4:7

i Isa 1:26

j Isa 49:26
Yer 50:18

Safu ya 2

a Ho 2:23

b Yer 31:1
Eze 11:20
Eze 36:28

c Yer 25:32

d Yer 4:28

e Yer 23:20

SURA YA 31

f Law 26:12
Yer 30:22
Yer 31:33

g Kum 7:8

h Yer 33:7
Amo 9:11

i Yer 30:18, 19

j Amo 9:14
Mik 4:4

- 22** “Nanyi mtakuwa watu wangu,^a nami nitakuwa Mungu wenu.”^b

- 23** Tazameni! Dhoruba ya Yehova ya upepo italipuka kwa ghadhabu,^c
Tufani inayofagia ambayo inazunguka ikishuka juu ya kichwa cha waovu.

- 24** Hasira inayowaka ya Yehova haitapoa
Mpaka atakapoteketeza na kutimiza makusudi ya moyo wake.^d
Mtaelewa jambo hilo kati-ka siku za mwisho.^e

- 31** “Wakati huo,” asema Yehova, “Nitakuwa Mungu wa familia zote za Israeli, nao watakuwa watu wangu.”^f

- 2** Yehova anasema hivi:
“Watu waliookoka upanga walipata kibali nyikani Israeli alipokuwa akitembea kwenda mahali pake pa kupumzika.”

- 3** Kutoka mbali Yehova alinitokea na kusema:
“Nimekupenda kwa upendo wa milele.

Ndiyo sababu nimekuvuta kwangu kwa upendo mshikamanifu.”^g

- 4** Kwa mara nyingine tena nitakujenga upya nawe utajengwa upya.^h
Ewe bikira wa Israeli, utachukua tena matari yako Na kwenda ukicheza dansi kwa shangwe.”ⁱ

- 5** Utapanda tena mashamba ya mizabibu kwenye milima ya Samaria;^j

31:3 *Au “nimeendelea kukutendea kwa upendo mshikamanifu.” **31:4** *Au “utaenda kucheza dansi ya wale wanaochecha.”

Wanaopanda watapanda
na kufurahia matunda
yake.^a

- 6** Kwa maana siku itafika
ambayo walinzi walio
kwenye milima ya Efraim-
mu watapaza sauti
wakisema:

‘Inukeni, twendeni juu Sa-
yuni, kwa Yehova Mungu
wetu.’^b

- 7** Kwa maana Yehova anase-
ma hivi:

“Mlilieni Yakobo kwa shan-
gwe.

Pigeni vigelegele vya shan-
gwe kwa sababu mko
juu ya mataifa.^c

Tangazeni jambo hilo; si-
funi na kusema,

‘Ee Yehova, waokoe watu
wako, Waisraeli wanao-
baki.’^d

- 8** Ninawarudisha kutoka
nchi ya kaskazini.^e
Nitawakusanya pamoja ku-
toka sehemu za mbali
zaidi za dunia.^f

Miongoni mwao kutakuwa
na vipofu na vilema,^g

Mwanamke mwenye mi-
mba na yule anayezaa,
wote pamoja.

Watarudi hapa wakiwa ku-
taniko kubwa.^h

- 9** Watakuja wakilia.ⁱ
Nitawaongoza huku wakio-
mba kibali.

Nitawaongoza kwenye viji-
to vya* maji.^j

Kwenye kijia tambarare
ambacho hakitawafanya
wajikwae.

Kwa maana mimi ni Baba
ya Israeli, naye Efraimu
ni mzaliwa wangu wa
kwanza.^k

31:9 *Au “makorongo ya.”

SURA YA 31

a Kum 30:9
Isa 65:21, 22

b Isa 2:3
Yer 50:4, 5

c Kum 32:43
Isa 44:23

d Isa 1:9
Yer 23:3
Yoe 2:32

e Isa 43:6
Yer 3:12

f Kum 30:4
Eze 20:34
Eze 34:12

g Isa 35:6
Isa 42:16

h Eze 2:1, 64

i Yer 50:4

j Isa 35:7
Isa 49:10

k Mwa 48:14
Kut 4:22

Safu ya 2

a Isa 11:11
Isa 42:10

b Isa 40:11
Eze 34:11-13
Mik 2:12

c Isa 44:23
Isa 48:20

d Isa 49:25

e Eze 3:13
Zb 126:1
Isa 51:11

f Yoe 3:18

g Isa 65:10

h Isa 58:11

i Isa 35:10

j Zek 8:4

k Eze 3:12

l Isa 51:3
Isa 65:19

m Kum 30:9
Isa 63:7

- 10** Sikieni neno la Yehova,
enyi mataifa,
Na mlitangaze kati ya visi-
wa vilivyo mbali sana:^a

“Yule aliyemtawanya
Israeli atamkusanya pa-
moja.

Atamlinda kama mchungu-
ji anavyochunga kundi
lake.^b

- 11** Kwa maana Yehova ata-
mkomboa Yakobo^c
Na kumwokoa* kutoka mi-
kononi mwa yule aliye na
nguvu zaidi yake.^d

- 12** Watakuja na kupiga vige-
legele vya shangwe juu
ya kilele cha Sayuni^e
Na kung’aa kwa sababu ya
wema wa* Yehova,
Kwa sababu ya nafaka na
divai mpya^f na mafuta,
Na kwa sababu ya wanako-
ndoo na ndama.^g

Watakuwa[#] kama bustani
iliyonyweshwa maji
vizuri,^h

Nao hawatadhoofika
tena.ⁱ

- 13** “Wakati huo bikira atache-
za dansi kwa shangwe,
Pia wanaume vijana na wa-
naume wazee pamoja.^j
Nitayageuza maombolezo
yao yawe furaha.^k
Nitawafaraji na kuwafanya
washangilie badala ya
kuhuzunika.^l

- 14** Nami nitawashibisha ma-
kuhani kwa vitu vingi,*
Na watu wangu watashiba
wema wangu,^m asema
Yehova.

31:11 *Au “kumkomboa.” 31:12 *Au
“vitu vizuri kutoka kwa.” #Au “Nafsi
yao itakuwa.” 31:14 *Tnn., “mafuta.”

- 15** “Yehova anasema hivi:
 ‘Sauti inasikika kule
 Rama,^a maombolezo na
 kilio cha uchungu:
 Raheli anawalilia
 wanawe.*^b
 Amekataa kufarijiwa ku-
 husiana na wanawe,
 Kwa sababu hawako
 tena.”^c
- 16** Yehova anasema hivi:
 “Zuia sauti yako usilie na
 macho yako yasitokwe
 na machozi,
 Kwa maana utapata tha-
 wabu kwa ajili ya kazi
 yako,’ asema Yehova.
 ‘Watarudi kutoka nchi ya
 adui.’^d
- 17** ‘Na kuna tumaini kwa ajili
 ya wakati wako ujao,’^e
 asema Yehova.
 ‘Wana wako watarudi
 kwenye eneo lao we-
 nyewe.”^f
- 18** “Hakika nimemsikia Efrai-
 mu akiomboleza,
 ‘Umenirekebisha, nami ni-
 merekebisha,
 Kama ndama ambaye haja-
 zoezwa.
 Nirudishe, nami nitageuka
 bila kusita,
 Kwa maana wewe ni Yeho-
 va Mungu wangu.
- 19** Kwa maana baada ya ku-
 geuka nilijuta;^g
 Baada ya kusaidiwa kue-
 lewa nilipiga paja langu
 kwa huzuni.
 Niliaibika na kufedhe-
 heka,^h
 Kwa maana nilibeba shu-
 tuma ya ujana wangu.”
- 20** “Je, Efraimu si mwana
 mwenye thamani

31:15 *Au “watoto wake.”

SURA YA 31

a Yos 18:21, 25
 Yer 40:1

b Omb 1:16

c Mt 2:16-18

d Ezz 1:5
 Yer 23:3
 Eze 11:17
 Ho 1:11

e Yer 29:11

f Yer 46:27

g Kum 30:1-3

h Ezz 9:6

Safu ya 2

a Yer 31:9
 Ho 14:4

b Ho 11:8

c Kum 32:36
 Mik 7:18

d Isa 62:10

e Isa 35:8

f Isa 1:26

g Zek 8:3

h Yer 33:12
 Eze 36:10, 11

i Zb 107:9

kwangu, au mtoto mpe-
 ndwa?^a

Kwa maana kila mara
 ninapomshutumu, bado
 ninamkumbuka.

Ndiyo sababu hisia zangu
 zimechochewa* kwa ajili
 yake.^b

Nami hakika nitamhuru-
 mia,” asema Yehova.^c

21 “Jiwekee alama za bara-
 bara,

Na uweke vibao vya
 ishara.^d

Kazia fikira barabara kuu,
 njia ambayo unapaswa
 kupitia.^e

Rudi, ewe bikira wa Israeli,
 rudi kwenye majiji haya
 yako.

22 Utaendelea kuyumba-
 yumba mpaka lini, ewe
 binti usiye mwaminifu?

Kwa maana Yehova ameu-
 mba jambo jipya duniani:
 Mwanamke atamtafuta
 mwanamume kwa bidii.”

23 Yehova wa majeshi, Mu-
 ngu wa Israeli, anasema hivi:
 “Watasema tena maneno haya
 katika nchi ya Yuda na ka-
 tika majiji yake nitakapowa-
 kusanya na kuwarudisha ma-
 teka wao: ‘Yehova na akuba-
 riki, Ee makao ya uadilifu,’^f
 Ee mlima mtakatifu.’^g **24** Na
 watu wa Yuda na majiji yake
 yote watakaa pamoja ndani
 yake, wakulima na wale wa-
 naochunga kondoo.^h **25** Kwa
 maana nitamshibisha aliye-
 choka na kumjaza kila mtu ali-
 yedhoofika.”ⁱ

26 Ndipo nikaamka na ku-
 fungua macho yangu, na usi-
 ngizi wangu ulikuwa mtamu.

31:20 *Tnn., “matumbo yangu yame-
 chochewa.”

27 “Tazama! Siku zinakuja,” asema Yehova, “nitakapopanda nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda kwa mbegu ya* mwanadamu na kwa mbegu ya mifugo.”^a

28 “Na kama nilivyowakazia uangalifu ili kuwang’oa, kuwabomoa, kuwaangusha, kuwaharibu, na kuwadhuru,^b ndivyo nitakavyowakazia uangalifu ili kuwajenga na kuwapanda,”^c asema Yehova.

29 “Katika siku hizo hawatasea tena, ‘Akina baba walikula zabibu chachu, lakini meno ya wana ndiyo yaliyotiwa ukakasi.’^{*d} 30 Lakini wakati huo kila mtu atakufa kwa sababu ya kosa lake mwenyewe. Mtu yeyote atakayekula zabibu chachu, atatiwa ukakasi kwenye meno yake mwenyewe.”

31 “Tazama! Siku zinakuja,” asema Yehova, “nitakapofanya agano jipya pamoja na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda.^e 32 Halitakuwa kama agano nililofanya pamoja na mababu zao siku niliyowashika mkono na kuwangoza kutoka nchini Misri,^f ‘agano langu ambalo walilivunja,^g ingawa nilikuwa bwana* wao wa kweli,’ asema Yehova.”

33 “Kwa maana hili ndilo agano nitakalofanya pamoja na nyumba ya Israeli baada ya siku hizo,” asema Yehova. “Nitaitia sheria yangu ndani yao,^h nami nitaiandika katika moyo wao.ⁱ Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.”^j

34 “Nao hawatafundishana tena kila mtu na jirani yake na

31:27 *Au “uzao wa.” 31:29 *Au “yaliyotiwa ganzi.” 31:32 *Au labda, “mume.”

SURA YA 31

a Kum 30:9
Eze 36:9
Ho 2:23

b Yer 44:27
Yer 45:4

c Zb 102:16
Zb 147:2
Yer 24:6

d Eze 18:2-4

e Mt 26:27, 28
Lu 22:20
1Ko 11:25
Ebr 8:8-12

f Kut 19:5

g Eze 16:59

h Eze 11:19

i Ebr 10:16

j Yer 24:7
Yer 30:22

Safu ya 2

a Isa 54:13
Yoh 17:3

b Isa 11:9
Hab 2:14

c Yer 33:8
Yer 50:20
Mt 26:27, 28
Ebr 8:10-12
Ebr 9:15
Ebr 10:17

d Isa 51:15

e Isa 54:10
Yer 33:20, 21

f Yer 30:11

g Ne 12:27
Isa 44:28
Yer 30:18

h Ne 3:1
Zek 14:10

i 2Nya 26:9

j Zek 1:16

k 2Sa 15:23
2Fa 23:6
Yoh 18:1

kila mtu na ndugu yake, waki-sema, ‘Mjue Yehova!’^a kwa maana wote watanijua, kuanzia mdogo zaidi mpaka mku-bwa zaidi kati yao,”^b asema Yehova. “Kwa maana nitalisamehe kosa lao, nami sitaikumbu-ka tena dhambi yao.”^c

35 Yehova,

Ambaye hutoa jua ili liangaze wakati wa mchana,

Sheria za* mwezi na nyota ili zianguwe usiku,

Anayetibua bahari na kuvavuruga mawimbi yake,

Ambaye jina lake ni Yehova wa majeshi, anasema hivi:^d

36 “‘Ikiwa sheria hizo zitakoma,’ asema Yehova, ‘Basi uzao wa Israeli utakoma daima kuwa taifa mbele zangu.’^e

37 Yehova anasema hivi: “‘Ikiwa mbingu zilizo juu zinaweza kupimwa na misingi ya dunia iliyo chini kuchungu-za, basi ninaweza kuukataa uzao wote wa Israeli kwa sababu ya yote ambayo wamefanya,’ asema Yehova.”^f

38 “Tazama! Siku zinakuja,” asema Yehova, “ambapo jiji litajengwa^g kwa ajili ya Yehova kutoka Mnara wa Hananeli^h mpaka Lango la Pembeni.ⁱ 39 Nayo kamba ya kupimia^j itaenda moja kwa moja mpaka kwenye kilima cha Garebu, nayo itageuka na kuelekea Goa. 40 Na bonde lote la mizoga na la* majivu,^k na matuta yote mpaka Bonde la Kidroni,^k mpaka kwenye pembe

31:35 *Au “Amri za.” 31:40 *Au “nchi yote tambarare ya chini ya mizoga na ya.” #Au “majivu yenye mafuta,” yaani, majivu yaliyojaa mafuta ya dhabihu.

ya Lango la Farasi^a kuelekea mashariki, litakuwa kitu kitakatifu kwa Yehova.^b Halitang'olewa tena kamwe wala kubomolewa.”

32 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova katika mwaka wa 10 wa utawala wa Mfalme Sedekia wa Yuda, yaani, mwaka wa 18 wa utawala wa Nebukadreza.*^c **2** Wakati huo majeshi ya mfalme wa Babiloni yalikuwa yakizingira Yerusalemu, naye nabii Yeremia alikuwa amezuiliwa katika Ua wa Walinzi^d katika nyumba ya* mfalme wa Yuda. **3** Kwa maana Mfalme Sedekia wa Yuda alikuwa amemzuilia,^e akisema: “Kwa nini unatabiri hivi? Unasema, ‘Yehova anasema hivi: “Nitalitia jiji hili mikononi mwa mfalme wa Babiloni, naye ataliteka,^f **4** na Mfalme Sedekia wa Yuda hataponyoka kutoka kwa Wakaldayo, kwa maana hakika atatiwa mikononi mwa mfalme wa Babiloni, naye atazungumza naye uso kwa uso na kumwona jicho kwa jicho.”^g **5** ‘Atampeleka Sedekia Babiloni, naye atakaa huko mpaka nitakapomkazia fikira,’ asema Yehova. ‘Ingawa mnaendelea kupigana na Wakaldayo, hamtafanikiwa.’”^h

6 Yeremia akasema: “Neno la Yehova limenijia likisema, **7** ‘Hanameli mwana wa Shalumu ndugu ya baba yako atakuja kwako na kukuambia: “Nunua shamba langu lililo Anathothi,ⁱ kwa sababu una haki ya kwanza ya kulikomboa.””^j

32:1 *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili. **32:2** *Au “jumba la.”

SURA YA 31

a Ne 3:28

b Yoe 3:17

SURA YA 32

c Yer 25:1

d Ne 3:25
Yer 33:1
Yer 38:28

e Yer 37:18, 21

f Yer 34:2, 3
Yer 37:8, 17g 2Fa 25:6, 7
Yer 38:17, 18
Yer 39:5
Eze 12:13h Yer 21:4
Eze 17:15i Yos 21:8, 18
Yer 1:1

j Law 25:23, 24

Safu ya 2

a Mwa 23:16

b Yer 32:44

c Ru 4:9

d Yer 36:4
Yer 36:26

e Yer 51:59

f Yer 33:1

8 Hanameli mwana wa ndugu ya baba yangu akaja kwangu, kama Yehova alivyo-sema, katika Ua wa Walinzi, naye akaniambia: “Tafadhali nunua shamba langu lililo Anathothi, katika nchi ya Benjamini, kwa maana una haki ya kulimiliki na kulikomboa. Linunue liwe lako.” Ndipo nikajua kwamba hilo lilikuwa neno la Yehova.

9 Basi nikalinunua shamba lililokuwa Anathothi kutoka kwa Hanameli mwana wa ndugu ya baba yangu. Nikampimia pesa,^a shekeli saba* na vipande kumi vya fedha. **10** Kisha nikaandika katika hati,^b nikaitia muhuri, nikawaita mashahidi,^c nami nikapima pesa kwa mizani. **11** Nikai-chukua ile hati ya ununuzi, ili-yotiwa muhuri kulingana na amri na masharti ya kishe-ria, na pia hati ambayo hai-kuwa na muhuri, **12** kisha nikampa hati hiyo ya ununuzi Baruku^d mwana wa Neriae mwana wa Mahseya mbele ya Hanameli mwana wa ndugu ya baba yangu, wale mashahidi walioandika kwenye hati ya ununuzi, na Wayahudi wote waliokuwa wameketi katika Ua wa Walinzi.^f

13 Sasa nikamwamuru Baruku mbele yao, nikisema: **14** “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Chukua hati hizi, hati hii ya ununuzi, iliyotiwa muhuri na ile hati nyingine isiyona muhuri, nawe uziweke katika chombo cha undogo, ili zihifadhiwe kwa muda mrefu.’ **15** Kwa maana Yehova wa ma-

32:9 *Shekeli moja ilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Angalia Nyongeza B14.

jeshi, Mungu wa Israeli, ana-sema hivi: 'Nyumba na mashamba na mashamba ya mizabibu yatanunuliwa tena katika nchi hii.'^a

16 Kisha nikasali kwa Yehova baada ya kumpa Baruku mwana wa Neria ile hati ya ununuzi, nikisema: **17** "Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Tazama! Uliumba mbingu na dunia kwa nguvu zako kuu^b na kwa mkono wako ulionyooshwa. Hakuna jambo la ajabu sana kwako, **18** Wewe unayewatendea kwa upendo mshikamanifu maelifu ya watu, lakini unawaadhibu wana kwa sababu ya makosa ya baba zao,^c Mungu wa kweli, uliye mkuu na Mwenye nguvu, ambaye jina lako ni Yehova wa majeshi. **19** Wewe ni mkuu katika kutoa mashauri* na matendo yako ni yenye nguvu,^d wewe ambaye macho yako huchunguza njia zote za wanadamu,^e ili kumlipa kila mtu kulingana na njia zake na matendo yake.^f **20** Ume-fanya ishara na miujiza katika nchi ya Misri, nayo inajulikana mpaka leo hii, na hivyo umejijengea jina katika Israeli na kati ya wanadamu,^g kama ilivyo leo. **21** Nawe uliwatoa watu wako Waisraeli nchini Misri, kwa ishara, kwa miujiza, kwa mkono wenye nguvu, kwa mkono ulionyooshwa, na kwa matendo yanayoogopesha.^h

22 "Baada ya muda ukawapa nchi hii ambayo uliapa kwamba utawapa mababu zao,ⁱ nchi inayotiririka maziwa na asali.^j **23** Nao wakai-

32:19 *Au "mkuu kuhusiana na makusudi yako."

SURA YA 32

a Amo 9:14
Zek 3:10

b Isa 40:26
Ufu 4:11

c Kut 34:6, 7
Hes 14:18

d Isa 28:29

e Met 15:3
Ebr 4:13

f Mhu 12:14
Yer 17:10
Ro 2:6

g Kut 7:3, 5
Kut 9:15, 16
Kum 4:34
2Sa 7:23
Isa 63:12

h Kut 6:1, 6
Kut 15:16
Kum 26:8

i Mwa 13:14, 15
Mwa 26:3

j Kut 3:8

Safu ya 2

a Kum 28:15
Yos 23:16

b Kum 28:52
2Fa 25:1
Yer 33:4
Eze 4:1, 2

c Law 26:31, 33

d Yer 14:12
Yer 15:2

e 2Fa 25:4
Yer 20:5

f 2Fa 25:9, 10
2Nya 36:17, 19
Omb 4:11

g Yer 7:18
Yer 19:13
Yer 44:25

h Kum 9:7
2Fa 17:9

ngia na kuimiliki, lakini hawakuitii sauti yako wala kumtembea katika sheria yako. Hawakufanya lolote kati ya mambo uliyowaamuru wafanye, hivi kwamba ukawaletea msiba huu wote.^a **24** Tazama! Watu wamekuja na maboma ya kuzingira ili kuliteka jiji hili,^b na kwa sababu ya upanga,^c njaa kali, na ugonjwa hatari,^d hakika jiji litaanguka mikononi mwa Wakaldayo wanaolishambulia; mambo uliyosema yametimia yote, kama unavyoona sasa. **25** Lakini umeniambia, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'Nunua shamba kwa pesa na uwaite mashahidi,' ingawa kwa hakika jiji litatiwa mikononi mwa Wakaldayo."

26 Ndipo neno la Yehova likamjia Yeremia likisema: **27** "Mimi ndimi, Yehova, Mungu wa wanadamu wote.* Je, kuna jambo lolote ambalo ni la ajabu sana kwangu? **28** Basi Yehova anasema hivi: 'Tazama, ninalitia jiji hili mikononi mwa Wakaldayo na mikononi mwa Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni, naye ataliteka.^e **29** Na Wakaldayo wanaolishambulia jiji hili wataingia na kuliteketeza^f pamoja na nyumba ambazo juu ya paa zake watu walimtolea dhabihu Baali na kuitolea miungu mingine matoleo ya kinywaji ili kunikasisisha.'^g

30 "Kwa maana watu wa Israeli na wa Yuda wame-tenda maovu tu machoni pangu, tangu ujana wao;^h watu wa Israeli wanaendelea

32:27 *Tnn., "wote wenye mwili wa nyama." **32:28** *Tnn., "Nebukadreza," njia nyingine ya kuandika jina hili.

kunikasirisha kwa kazi ya mkono yao,' asema Yehova. **31** 'Kwa maana jiji hili, tangu siku walipolijenga mpaka leo hii, limekuwa tu likinikasirisha na kunitia ghadhabu,^a hivi kwamba ni lazima liondolewe mbele za uso wangu,^b **32** kwa sababu ya uovu wote ambao watu wa Israeli na wa Yuda walifanya ili kunikasirisha—wao, wafalme wao,^c wakuu wao,^d makuhani wao, manabii wao,^e na watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu. **33** Waliendelea kunigeuzia migongo yao, si nyuso zao;^f ingawa nilijaribu kuwafundisha tena na tena,* hakuna hata mmoja wao aliyesikiliza ili kupokea nidhamu.^g **34** Nao waliweka sanamu zao zinazochukiza katika nyumba inayoitwa kwa jina langu, ili kuitia unajisi.^h **35** Isitoshe, walijenga mahali pa juu pa Baali katika Bonde la Mwana wa Hinomu,ⁱ ili kuwatekeleza[#] motoni wana wao na mabinti wao kwa ajili ya Moleki,^j jambo ambalo sikuwaamuru,^k na ambalo halijawahi kamwe kuingia moyoni mwangu,^Δ kufanya jambo hilo linalochukiza, na kusababisha watu wa Yuda watende dhambi.'

36 "Kwa hiyo Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi kuhusu jiji hili ambalo mnasema litatiwa mikononi mwa mfalme wa Babiloni kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari, **37** 'Nitawakusanya pamoja kutoka katika nchi zote ambako niliwatawanyanya kwa hasira yangu

32:33 *Tnn., "kuamka mapema na kuwafundisha." **32:35** *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Gehena." #Tnn., "kuwapitisha." ΔAu "sijawahi kamwe kulifikiria."

SURA YA 32

- a 1Fa 11:7
2Fa 21:1, 4
b 2Fa 23:27
2Fa 24:3, 4
c 1Fa 11:9, 10
2Fa 23:26
1Nya 10:13
d Eze 22:6
e Mik 3:5, 11
f 2Nya 29:6
Yer 2:27
g Yer 25:3
Yer 35:15
h 2Fa 21:1, 4
Yer 23:11
Eze 8:5, 6
i Yos 15:8, 12
j 2Nya 28:1, 3
2Nya 33:1, 6
Yer 7:31
k Law 18:21
Kum 18:10, 12

Safu ya 2

- a Kum 30:3
Yer 29:14
Eze 37:21
b Yer 23:3, 6
Yer 33:16
Eze 34:25
c Yer 31:33
Mik 4:5
d Eze 11:19
e Kum 5:29
f Isa 55:3
Isa 61:8
g Eze 39:29
h Eze 36:26
i Isa 65:19
Sef 3:17
j Isa 58:11
Yer 24:6
Amo 9:15
k Yer 31:28
Zek 8:14, 15
l Eze 37:14
m Yer 32:10, 25
n Yer 31:23

- o Yer 17:26
Yer 33:13
p Zb 126:1

na kwa ghadhabu yangu na kwa ukali mwingi,^a nami nitawarudisha mahali hapa na kufanya wakae kwa usalama.^b **38** Nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao.^c **39** Nami nitawapa moyo mmoja^d na njia moja ili waniogope sikuzote, kwa faida yao wenyewe na kwa faida ya watoto wao baada yao.^e **40** Nami nitafanya pamoja nao agano linalodumu milele,^f kwamba sitaacha kuwatendea mema;^g nami nitatia hofu yangu katika mioyo yao, hivi kwamba hawataniacha.^h **41** Nitafurahia kuwatendea mema,ⁱ nami nitawapanda kwa uthabiti katika nchi hii,^j kwa moyo wangu wote na kwa nafsi* yangu yote."

42 "Kwa maana Yehova anasema hivi: 'Kama nilivyo-waleta watu hawa msiba huu mkubwa, ndivyo nitakavyo-waleta mema yote ninayo-waahidi.*^k **43** Na mashamba yatanunuliwa tena katika nchi hii,^l ingawa mnasema: "Ni nchi yenye ukiwa isiyo na mwanadamu wala mnyama, nayo imetiwa mikononi mwa Wakaldayo."

44 "Mashamba yatanunuliwa kwa pesa, hati za ununuzi zitaandikwa na kutiwa muhuru, nao mashahidi wataitwa katika nchi ya Benjamini,^m katika maeneo yanayozunguka Yerusalemu, katika majiji ya Yuda,ⁿ katika majiji ya eneo lenye milima, na katika majiji ya eneo la chini,^o na katika majiji ya kusini, kwa sababu nitawarudisha mateka wao,^p asema Yehova."

32:41 *Angalia Kamusi, uku. 2012. **32:42** *Au "vitu vyote vizuri ninavyo-waahidi."

33 Neno la Yehova likamjia Yeremia mara ya pili, alipokuwa bado amezuiliwa katika Ua wa Walinzi,^a na kusema: **2** “Yehova, Muumba wa dunia, anasema hivi, Yehova aliyeiumba na kuifanya imara kabisa; Yehova ndilo jina lake, **3** ‘Niite, nami nita-kujibu na kukuambia kwa utayari mambo makubwa na ya-siyoeleweka ambayo hujayajua.’”^b

4 “Kwa maana Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi kuhusu nyumba za jiji hili na kuhusu nyumba za wafalme wa Yuda ambazo zimebomolewa kwa sababu ya maboma ya kuzingira na kwa sababu ya upanga,^c **5** na kuhusu wale wanaokuja kupigana na Wakaldayo, na kujaza maeneo haya mizoga ya wale niliowaua katika hasira yangu na katika ghadhabu yangu, wale ambao uovu wao umenifanya niufiche uso wangu kutoka kwenye jiji hili: **6** ‘Ninamponya na kumpa afya,^d nami nitawaponya na kuwafunulia wingi wa amani na kweli.’^e **7** Nami nitawarudisha mateka wa Yuda na mateka wa Israeli,^f nami nitawajenga kama nilivyofanya mwanzoni.^g **8** Nami nitawatakasa kutokana na hatia yote ya dhambi walizonitendea,^h nami nitasamehe hatia yote ya dhambi zao na makosa waliyonikosea.ⁱ **9** Naye atakuwa kwangu jina la furaha, sifa, na uzuri mbele ya mataifa yote ya dunia yatakayosikia kuhusu wema wote nitakaowapa.^j Nao wataogopa na kutetemeka^k kwa sababu ya wema na amani ninayompa.”^l

SURA YA 33

a Ne 3:25
Yer 32:2
Yer 37:21
Yer 38:28

b Isa 48:6

c Kum 28:52
Yer 32:24

d Isa 30:26
Yer 30:17

e Isa 54:13

f Kum 30:3
Yer 30:3

g Yer 24:6

h Isa 40:2
Zek 13:1

i Zb 85:2
Isa 43:25
Yer 31:34
Mik 7:18

j Isa 62:3, 7

k Mik 7:17

l Ne 6:15, 16

Safu ya 2

a Yer 31:12

b Zek 9:17

c 2Nya 5:13
Ezr 3:11
Zb 106:1
Isa 12:4
Mik 7:18

d Law 7:12
Zb 107:22

e Isa 65:10
Yer 32:43

f Yer 17:26

g Yer 32:44

h Yer 29:10

i Isa 53:2
Zek 6:12
Ufu 22:16

j Isa 11:1, 4
Yer 23:5
Ebr 1:9

10 “Yehova anasema hivi, ‘Mahali hapa ambapo mtasema ni nchi iliyo ukiwa, isiyo na wanadamu wala mifugo, katika majiji ya Yuda na katika barabara za Yerusalemu zilizo tupu, bila wanadamu wala wakaaji wala mifugo, itasikika tena **11** sauti ya furaha na sauti ya shangwe,^a sauti ya bwana harusi na sauti ya bibi harusi, sauti ya wale wanaosema: “Mshukuruni Yehova wa majeshi, kwa maana Yehova ni mwema;^b upendo wake mshikamanifu unadumu milele!”^c

“Wataleta matoleo ya shukrani katika nyumba ya Yehova,^d kwa maana nitawarudisha mateka wa nchi, kama hapo mwanzoni,’ asema Yehova.”

12 “Yehova wa majeshi anasema hivi, ‘Katika eneo hili lenye ukiwa, lisilo na mtu au mifugo, na katika majiji yake yote kutakuwa tena na malisho kwa ajili ya wachungaji kupumzisha makundi yao.’^e

13 “Katika majiji ya eneo lenye milima, katika majiji ya eneo la chini, katika majiji ya kusini, katika nchi ya Benjamin, katika maeneo yanayozunguka Yerusalemu^f na katika majiji ya Yuda,^g makundi yatapita tena chini ya mikono ya mtu anayeahesabu,^h asema Yehova.”

14 “Tazama! Siku zinakuja,ⁱ asema Yehova, ‘nitakapotimiza ahadi nzuri niliyotoa kuhusu nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda.’^h **15** Siku hizo na wakati huo nitamchipushia Daudi chipukizi adilifu,^{*i} naye atatenda haki na uadilifu katika nchi.^j **16** Siku

33:15 *Au “mrithi mwadilifu.”

hizo Yuda ataokolewa^a na Yerusalemu litakaa katika usalama.^b Naye ataitwa: Yehova Ni Uadilifu Wetu.”^c

17 “Kwa maana Yehova anasema hivi, ‘Hutakosa kamwe mwanamume wa ukoo wa Daudi atakayeketi kwenye kiti cha ufalme cha nyumba ya Israeli,^d **18** wala makuhani Walawi hawatakosha mtu wa kusimama mbele zangu ili kutoa dhabihu nzima za kutekeleza, kuchoma matoleo ya nafaka, na kutoa dhabihu.”

19 Nalo neno la Yehova likamjia Yeremia tena, na kusema: **20** “Yehova anasema hivi, ‘Ikiwa mngeweza kulivunja agano langu kuhusu mchana na agano langu kuhusu usiku, ili kuzuia mchana na usiku usije kwa wakati wake,^e **21** hapo ndipo agano langu pamoja na mtumishi wangu Daudi lingeweza kuvunjwa,^f ili asiwe na mwana anayetawala akiwa mfalme kwenye kiti chake cha ufalme,^g na pia agano langu pamoja na makuhani, Walawi, wahudumu wangu.^h **22** Kama jeshi la mbinguni lisivyoweza kuhesabiwa wala mchanga wa bahari usivyoweza kupimwa, ndivyo nitakavyozidisha uzao wa* mtumishi wangu Daudi na Walawi wanaonihudumia.”

23 Nalo neno la Yehova likamjia tena Yeremia, na kusema: **24** “Je, hujasikia yale ambayo watu hawa wanasema, ‘Yehova atazikataa familia mbili alizozichagua?’ Nao wanawavunja heshima watu wangu, na hawawatambui tena kuwa taifa.

33:22, 26 *Tnn., “mbegu ya.”

SURA YA 33

a Isa 45:17

b Eze 28:26

c Yer 23:6

d 2Sa 7:16, 17
1Fa 2:4
Zb 89:20, 29
Isa 9:7
Lu 1:32, 33

e Mwa 1:16
Isa 54:10
Yer 31:35-37

f 2Sa 7:16, 17
2Sa 23:5
Zb 89:34, 35
Zb 132:11
Isa 55:3

g Isa 9:6
Lu 1:32, 33

h Kum 21:5

Safu ya 2

a Mwa 1:16

b Zb 104:19
Yer 31:35, 36

c Eze 2:1, 70

d Isa 14:1
Yer 31:20

SURA YA 34

e 2Fa 25:1
Yer 32:2
Yer 39:1
Yer 52:4

f 2Nya 36:11
Yer 37:1

g Yer 21:10
Yer 32:28, 29
Yer 39:8

h Yer 37:17
Yer 39:5

i 2Fa 25:6, 7
Eze 12:13

j Eze 17:16

25 “Yehova anasema hivi: ‘Kwa hakika kama nilivyoweka imara agano langu kuhusu mchana na usiku,^a sheria za* mbingu na dunia,^b **26** vi-vyo hivyo sitaukataa kamwe uzao wa* Yakobo na wa mtumishi wangu Daudi, hivi kwamba nisichukue kutoka kwa uzao wake^c watawala wa wazao wa* Abrahamu, Isaka, na Yakobo. Kwa maana nita-wakusanya mateka wao^c na kuwahurumia.”^d

34 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova, Mfalme Nebukadnezah* wa Babiloni na jeshi lake lote na falme zote za dunia chini wa mamlaka yake na mataifa yote yalipokuwa yakishambulia Yerusalemu na majiji yake yote:^e

2 “Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Nenda uzungumze na Mfalme Sedekiah* wa Yuda nawe umwambie hivi: “Yehova anasema, ‘Ninalitia jiji hili mikononi mwa mfalme wa Babiloni, naye ataliteketeza kwa moto.^g **3** Nawe hutaponyoka kutoka mikononi mwake, kwa maana kwa hakika utakamatwa na kutiwa mikononi mwake.^h Nawe utamwona Mfalme wa Babiloni jicho kwa jicho, naye atazungumza nawe uso kwa uso, nawe utapeleka Babiloni.”ⁱ **4** Hata hivyo, sikia neno la Yehova, ewe Mfalme Sedekiah* wa Yuda, ‘Yehova anasema hivi kukuhusu wewe: “Hutakufa kwa upanga. **5** Utakufa kwa amani,^j nao watakufanyia sherehe ya kufukiza

33:25 *Au “amri za.” 33:26 #Tnn., “mbegu yake.” 34:1 *Tnn., “Nebukadrezah,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

manukato kama walivyowafanyia baba zako, wafalme wa zamani waliokutangulia, nao watakuombolezea wakisema, 'Ole, ewe bwana!' kwa maana 'nimelisema neno hilo,' asema Yehova. "''''"

6 Kisha nabii Yeremia akamwambia maneno haya yote Mfalme Sedekia wa Yuda huko Yerusalemu, **7** majeshi ya mfalme wa Babiloni yalipokuwa yakishambulia Yerusalemu na majiji yote ya Yuda yaliyobaki,^a yakishambulia Lakishi^b na Azeka;^c kwa maana hayo ndiyo majiji pekee ya Yuda yenye ngome yaliyobaki.

8 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova baada ya Mfalme Sedekia kufanya agano pamoja na watu wote waliokuwa Yerusalemu ili kuwatangazia uhuru,^d **9** kwa kamba kila mtu awaachilie huru watumwa wake Waebrania, wa kiume na wa kike, ili mtu yeyote asimfanye Myahudi mwenzake kuwa mtumwa. **10** Basi wakuu wote na watu wote wakatii. Walikuwa wamefanya agano kwamba kila mtu awaachilie huru watumwa wake wa kiume na wa kike na asiwafanye tena kuwa watumwa. Wakatii na kuwaruhusu waende zao. **11** Hata hivyo, baadaye waliwarudisha watumwa wao wa kiume na wa kike ambao walikuwa wamewaaachilia huru, nao wakawalazimisha tena kuwa watumwa. **12** Basi neno la Yehova likamjia Yeremia kutoka kwa Yehova likisema:

13 "Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: 'Nili-fanya agano pamoja na mababu zenu' siku niliyowatoa nchini Misri, kutoka katika

SURA YA 34

a Yer 4:5

b Mik 1:13

c Yos 15:20, 35

d Kut 21:2

e Kut 24:7

Safu ya 2

a Kut 13:3

b Kut 21:2
Law 25:10
Law 25:39-42
Kum 15:12

c Law 19:12

d Kut 21:2
Law 25:10

e 2Fa 25:3
Yer 21:7

f Yer 15:2, 4
Yer 29:18

g Mwa 15:10, 17

nyumba ya utumwa,^a nikisema: **14** "Mwishoni mwa miaka saba, kila mmoja wenu anapaswa kumwachilia huru ndugu yake Mwebrania aliyeuwza kwake na ambaye ametumikia miaka sita; lazima umwachilie huru."^b Lakini mababu zenu hawakunisikiliza wala kunitegea masikio yao. **15** Na hivi karibuni* ninyi wenyewe mligeuka na kufanya yaliyo sawa machoni pangu kwa kuwatangazia uhuru wenzenu, nanyi mkafanya agano mbele zangu katika nyumba inayoitwa kwa jina langu. **16** Lakini mligeuka tena na kulichafua jina langu^c kwa kuwarudisha watumwa wenu wa kiume na wa kike ambao mlikuwa mmewaachilia huru kama walivyotaka, nanyi mkawalazimisha tena kuwa watumwa.'

17 "Kwa hiyo Yehova anasema hivi: 'Hamjanitii kwa sababu kila mtu hajamtangazia uhuru ndugu yake na mwenzake.^d Basi sasa ninawatangazia uhuru,' asema Yehova, 'kwa upanga, ugonjwa hatari, na njaa kali,^e nami nitawafanya muwe kitu cha kutisha kwa falme zote za dunia.^f **18** Na hivi ndivyo itakavyokuwa kwa watu waliolivunja agano langu kwa kutofuata maneno ya agano walilofanya mbele zangu walipomkata ndama vipande viwili na kupita kati ya vile vipande viwili,^g **19** yaani, wakuu wa Yuda, wakuu wa Yerusalemu, maofisa wa makao ya mfalme, makuhani, na watu wote wa nchi waliopita kati ya vile vipande viwili vya ndama:

34:15 * Tnn., "leo."

20 Nitawatia mikononi mwa maadui wao na mikononi mwa wale wanaotaka kuwaua,* na maiti zao zitakuwa chakula cha ndege wa angani na cha wanyama wa dunia.^a

21 Nami nitamtia Mfalme Sedekia wa Yuda na wakuu wake mikononi mwa maadui wao na mikononi mwa wale wanaotaka kuwaua* na mikononi mwa majeshi ya mfalme wa Babiloni,^b ambao wanaondoka na kuacha kuwashambulia.^c

22 “Nitatoa agizo,’ asema Yehova, ‘nami nitawarudisha katika jiji hili, nao watalishambulia na kuliteka na kuliteketeza kwa moto;^d nami nitayafanya majiji ya Yuda yawe ukiwa, bila mkaaji.”^e

35 Neno lililomjia Yere-mia kutoka kwa Yehova katika siku za Yehoyakimu^f mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda likisema: **2** “Nenda katika nyumba ya Warekabu^g na uzungumze nao na kuwaleta katika nyumba ya Yehova, katika mojawapo ya vyumba vya kulia chakula;* nawe uwape divai wanywe.”

3 Basi nikampeleka Yaazania mwana wa Yeremia mwana wa Habasania, ndugu zake, wanawe wote, na nyumba yote ya Warekabu **4** kwenye nyumba ya Yehova. Niliwapeleka katika chumba cha kulia chakula cha wana wa Hani mwana wa Igdalia, mtu wa Mungu wa kweli, kilichokuwa kando ya chumba cha kulia chakula cha wakuu ambacho kilikuwa juu ya chumba cha kulia chakula cha Maaseya mwana wa Shalumu mlnzi

34:20, 21 *Au “wanaotafuta nafsi zao.”
35:2 *Au “vile vyumba.”

SURA YA 34

a Kum 28:26
Zb 79:2
Yer 16:4

b 2Fa 25:6, 7
Omb 4:20

c Yer 37:5

d 2Fa 25:9, 10
Yer 32:29
Yer 39:8

e Law 26:33
Yer 44:2

SURA YA 35

f 2Fa 23:34
2Nya 36:5
Da 1:1

g 2Fa 10:15
1Nya 2:55

Safu ya 2

a 2Fa 10:15

b 2Nya 36:5, 6
Da 1:1

wa mlango. **5** Kisha nikawe-ka vikombe na bilauri zilizojaa divai mbele ya watu wa nyumba ya Warekabu na kuwaambia: “Kunyweni divai.”

6 Lakini wakasema: “Hatutakunywa divai, kwa sababu Yehonadabu*^a mwana wa Rekabu, babu yetu, alituamuru hivi: ‘Ninyi wala wana wenu hampaswi kamwe kunywa divai. **7** Nanyi hampaswi kujenga nyumba, kupanda mbegu, au kupanda shamba la mizabibu au kulimiliki. Badala yake, mnapaswa kukaa katika mahema sikuzote, ili mwishi kwa muda mrefu katika nchi mnayoishi ndani yake mkiwa wageni.’ **8** Basi tunaendelea kuitii sauti ya Yehonadabu mwana wa Rekabu babu yetu kuhusu mambo yote aliyotumuru, kwa kutokunywa kamwe divai—sisi, wake zetu, wana wetu, na mabinti wetu. **9** Nasi hatujengi nyumba za kuishi humo, wala hatuna mizabibu wala mashamba wala mbegu. **10** Tunaendelea kuishi katika mahema na kutii mambo yote ambayo babu yetu Yehonadabu* alituamuru. **11** Lakini Mfalme Nebukadreza* wa Babiloni alipoishambulia nchi,^b tukasema, ‘Njooi, tuingie ndani ya Yerusalemu ili kuepuka jeshi la Wakaldayo na la Wasiria, na sasa tunaishi Yerusalemu.’”

12 Na neno la Yehova likamjia Yeremia likisema: **13** “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Nenda uwaambie watu

35:6, 10 *Tnn., “Yonadabu,” ufupisho wa jina Yehonadabu. 35:11 *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu: “Je, hamkuendelea kuhimizwa myatii maneno yangu?”^a asema Yehova. **14** “Yehonadabu mwana wa Rekabu aliwaamuru wazao wake wasinywe divai, nao wamefuata maneno yake kwa kutokunywa divai mpaka leo hii, na hivyo wameitii amri ya babu yao.^b Hata hivyo, nimezungumza nanyi tena na tena,* lakini hamjaitii.^c **15** Nami niliendelea kuwatuma kwenu watumishi wangu wote manabii, nikiwatumia tena na tena,*^d na kusema, ‘Tafadhali geukeni, kila mmoja wenu kuoka kwenye njia zenu za uovu,^e nanyi mfaneye yaliyo sawa! Msifuate miungu mingine na kuiabudu. Ndipo mtakapoendelea kukaa katika nchi niliyowapa ninyi na mababu zenu.’^f Lakini hamkutega sikio lenu wala hamkunisikiliza. **16** Wazao wa Yehonadabu mwana wa Rekabu wamefuata agizo ambalo babu yao aliwapa,^g lakini watu hawa hawajanisikiliza.”

17 “Kwa hiyo Yehova, Mungu wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Nina-waletea watu wa Yuda na wakaaji wote wa Yerusalemu msiba wote niliowaonya kuu-husu,^h kwa maana nimezungumza nao, lakini walikataa kusikiliza, nami nikaendelea kuwaita, lakini walikataa kujibu.’”ⁱ

18 Naye Yeremia akawaambia hivi watu wa nyumba ya Warekabu: “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anase-

35:14 *Tnn., “niliamka mapema na kuzungumza nanyi.” **35:15** *Tnn., “nikiamka mapema na kuwatuma.”

SURA YA 35

a Yer 32:33

b Yer 35:8

c 2Nya 36:15, 16
Ne 9:26, 30
Yer 25:3

d Yer 7:24, 25

e Isa 1:16
Yer 25:5
Eze 18:30
Ho 14:1

f Yer 7:5-7

g Yer 35:8

h Kum 28:15
Kum 29:26, 27
Yos 23:15, 16
2Fa 23:27i Isa 65:12
Isa 66:4
Yer 7:13, 14

Safu ya 2

SURA YA 36

a 2Fa 23:36
Yer 25:1b Yer 4:16
Yer 32:30c Yer 1:5
Yer 25:9d Yer 1:1, 2
Yer 25:3e Isa 55:7
Eze 33:11
Mik 7:18f Yer 32:12
Yer 45:2-5

g Yer 45:1

ma hivi: ‘Kwa sababu mmetii agizo la babu yenu Yehonadabu nanyi mnaendelea kufuata maagizo yake yote, na kufanya sawasawa na alivyo-waagiza, **19** Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Hatakosekana kamwe mzao wa Yehonadabu* mwana wa Rekabu atakayetu-mikia mbele zangu.””

36 Sasa katika mwaka wa nne wa utawala wa Yehoyakimu^a mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, neno hili lilimjia Yeremia kutoka kwa Yehova likisema: **2** “Chukua kitabu cha kukunjwa na uandike ndani yake maneno yote ambayo nimekuambia dhidi ya Israeli na Yuda^b na mataifa yote,^c tangu siku ya kwanza niliyozungumza nawe katika siku za utawala wa Yosia mpaka leo hii.^d **3** Labda watu wa nyumba ya Yuda watakaposikia kuhusu msiba wote ninaokusudia kuwaletea, wataziacha njia zao za uovu, ili niwasamehe kosa lao na dhambi yao.”^e

4 Kisha Yeremia akamwita Baruku^f mwana wa Neria, naye Yeremia akamwambia maneno yote ambayo Yehova alikuwa amemwambia, naye Baruku akayaandika maneno hayo katika kitabu cha kukunjwa Yeremia alipokuwa akiyasema.^g **5** Kisha Yeremia akamwamuru Baruku: “Nimezuliwa, siwezi kuingia katika nyumba ya Yehova. **6** Basi wewe ndiye utakayeingia na kusoma kwa sauti maneno ya Yehova yaliyo katika kitabu cha kukunjwa

35:19 *Tnn., “Yonadabu,” ufupisho wa jina Yehonadabu.

ulichoandika nilipokuwa nikiyasema. Yasome watu wakisia katika nyumba ya Yehova siku ya kufunga; basi utawasomea watu wote wa Yuda wanaokuja kutoka katika majiji yao. **7** Labda ombi lao la kutaka kibali litamfikia Yehova, nao watageuka, kila mtu kutoka katika njia zake za uovu, kwa maana Yehova amewatangiata watu hawa hasira na ghadhabu kubwa.”

8 Basi Baruku mwana wa Neria akafanya yote ambayo nabii Yeremia alimwamuru; akasoma kwa sauti maneno ya Yehova yaliyokuwa katika kile kitabu cha kukunjwa kwenye nyumba ya Yehova.^a

9 Katika mwaka wa tano wa utawala wa Yehoyakimu^b mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, katika mwezi wa tisa, watu wote wa Yerusalemu na watu wote waliokuja Yerusalemu kutoka katika majiji ya Yuda wakatanga watu wafunge mbele za Yehova.^c **10** Kisha Baruku akasoma kwa sauti maneno ya Yeremia yaliyokuwa katika kile kitabu cha kukunjwa kwenye nyumba ya Yehova, katika chumba* cha Gemaria^d mwana wa Shafani^e mwandishi,^f katika ua wa juu, kwenye njia inayoelekea kwenye lango jipya la nyumba ya Yehova,^f watu wote wakisia.

11 Mikaya mwana wa Gemaria mwana wa Shafani alipoyasikia maneno yote ya Yehova kutoka katika kile kitabu cha kukunjwa, **12** akashuka kwenda kwenye nyumba ya* mfalme, katika chumba cha

SURA YA 36

a Yer 7:1, 2

b 2Fa 23:36

c 2Nya 20:2, 3
Est 4:15, 16

d Yer 36:25

e 2Fa 22:8
2Nya 34:20, 21
Yer 26:24
Yer 39:13, 14
Eze 8:11

f Yer 26:10

Safu ya 2

a Yer 36:20

b Yer 36:25

c 2Fa 22:14
Yer 26:22

d Yer 36:26

mwandishi. Wakuu wote* walikuwa wameketi humo: mwandishi Elishama,^a Delaya mwana wa Shemaya, Elnathani^b mwana wa Akbori,^c Gemaria mwana wa Shafani, Sedekia mwana wa Hanania, na wakuu wengine wote. **13** Mikaya akawaambia maneno yote aliyokuwa ameyasikia Baruku aliposoma kile kitabu cha kukunjwa mbele ya watu.

14 Ndipo wakuu wote waka mtuma Yehudi mwana wa Nethania mwana wa Shelemia mwana wa Kushi kwa Baruku, wakisema: “Njoo na kitabu cha kukunjwa ulichosoma mbele ya watu.” Baruku mwana wa Neria akabeba kile kitabu cha kukunjwa mkononi mwake na kuingia walimokuwa. **15** Wakamwambia: “Tafadhali keti, nawe utusomee kitabu hicho kwa sauti.” Basi Baruku akawasomea kitabu hicho.

16 Sasa mara tu walipoyasikia maneno hayo yote, wakaangaliana kwa hofu, nao wakamwambia Baruku: “Lazima tumwambie mfalme maneno haya yote.” **17** Nao wakamuuliza Baruku: “Tafadhali tuambie jinsi ulivyoandika maneno haya yote. Je, aliyasema huku ukiandika?” **18** Baruku akawajibu: “Ali niambia maneno haya yote, nami nikayaandika kwa wino katika kitabu hiki cha kukunjwa.” **19** Wakuu wakamwambia Baruku: “Nenda ujifiche, wewe pamoja na Yeremia, na msiache mtu yeyote ajue mahali mlipo.”^d

36:12 *Au “Maofisa wote wa makao ya mfalme.”

36:10 *Au “chumba cha kulia chakula.”

^aAu “aliyenakili maandishi.” **36:12** *Au “jumba la.”

20 Kisha wakaingia kwa mfalme, kwenye ua, na ku-kiweka kitabu hicho cha kukunjwa kwenye chumba cha mwandishi Elishama, nao wakamwambia mfalme kila kitu walichosikia.

21 Basi mfalme akamtuma Yehudi^a aende kuleta kitabu hicho cha kukunjwa, naye akakileta kutoka katika chumba cha mwandishi Elishama. Yehudi akaanza kukisoma mbele ya mfalme na wakuu wote waliokuwa wamesimama karibu na mfalme. **22** Mfalme alikuwa ameketi katika nyumba ya majira ya baridi kali, katika mwezi wa tisa,* huku jiko la makaa likiwaka mbele yake. **23** Kila mara Yehudi aliposoma safu tatu au nne, mfalme alikata sehemu hiyo kwa kisu cha mwandishi na kuitupa ndani ya moto katika jiko la makaa, mpaka kitabu chote cha kukunjwa kilipoteketea katika jiko hilo. **24** Nao hawakushikwa na hofu yoyote; wala mfalme wala watumishi wake wote waliosikia maneno hayo hawakuyararua mavazi yao. **25** Ingawa Elnathani,^b Delaya,^c na Gemaria^d walimsihi mfalme asikiteketee kitabu hicho cha kukunjwa, hakuwasikiliza. **26** Isitoshe, mfalme akawaamuru Yerahmeeli mwana wa mfalme, Seraya mwana wa Azrieli, na Shelemia mwana wa Abdeeli wamkamate mwandishi Baruku na nabii Yeremia, lakini Yehova akaendelea kuwaficha.^e

27 Na neno hili la Yehova likamjia Yeremia tena baada ya

36:22 *Nusu ya pili ya Novemba na nusu ya kwanza ya Desemba. Angalia Nyongeza B15.

SURA YA 36

a Yer 36:14

b 2Fa 24:8

c Yer 36:12

d Yer 36:10

e Yer 1:19

Safu ya 2

a Yer 36:2

b Yer 36:23

c Yer 25:8, 9

d 2Fa 24:6, 8
2Fa 24:15
2Nya 36:9, 10
Yer 22:24, 30

e Yer 22:18, 19

f Kum 28:15
Yer 19:15

g 2Nya 36:15, 16

h Yer 36:2, 4

mfalme kukiteketeeza kile kitabu cha kukunjwa kilichokuwa na maneno ambayo Baruku aliyaandika Yeremia alipokuwa akiyasema:^a **28** "Chukua kitabu kingine cha kukunjwa nawe uandike ndani yake maneno yaleyale yaliyokuwa kwenye kile kitabu cha kwanza cha kukunjwa, ambacho Mfalme Yehoyakimu wa Yuda alikiteketeeza.^b **29** Nawe unapaswa kusema hivi dhidi ya Mfalme Yehoyakimu wa Yuda: 'Yehova anasema hivi: "Ume- kiteketeeza kitabu hiki cha kukunjwa na kusema, 'Kwa nini umeandika ndani yake, "Mfalme wa Babiloni atakuja hakika na kuiharibu nchi hii na kumwangamiza mwanadamu na mnyama kutoka humu?"^c

30 Kwa hiyo Yehova anasema hivi dhidi ya Mfalme Yehoyakimu wa Yuda, 'Hatakuwa na mtu yeyote atakayeketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi,^d na maiti yake itaachwa nje kwenye joto wakati wa mchana na baridi kali wakati wa usiku.^e **31** Nitamwadhibu yeye na wazao wake* na watumishi wake kwa sababu ya kosa lao, nami nitawaletea wao na wakaaji wa Yerusalemu na watu wa Yuda msiba wote niliotangaza dhidi yao,^f lakini hawakusikiliza."^g

32 Kisha Yeremia akachukua kitabu kingine cha kukunjwa na kumpa Baruku mwana wa Neria, mwandishi,^h naye akaandika maneno yote aliyambiwa na Yeremia ambayo yalikuwa katika kile kitabu cha kukunjwa ambacho Mfalme Yehoyakimu wa Yuda

36:31 * Tnn., "mbegu yake."

alikuwa amekitekeza motoni.^a Na maneno mengine mengi kama hayo yakaongezwa.

37 Na Mfalme Sedekia^b mwana wa Yosia akaanza kutawala baada ya Konia^{*c} mwana wa Yehoyakimu, kwa maana Mfalme Nebukadneza[#] wa Babiloni alikuwa amemweka kuwa mfalme katika nchi ya Yuda.^d **2** Lakini yeye na watumishi wake na watu wa nchi hawakuyasikiliza maneno ya Yehova yaliyosemwa kupitia nabii Yeremia.

3 Na Mfalme Sedekia akamtuma Yehukali^e mwana wa Shelemia na Sefania^f mwana wa kuhani Maaseya kwa nabii Yeremia, akisema: “Tafadhali sali kwa ajili yetu kwa Yehova Mungu wetu.” **4** Yeremia alikuwa akitembea kwa uhuru miongoni mwa watu, kwa maana bado hakuwa ametiwa gerezani.^g **5** Sasa jeshi la Farao lilikuwa limeondoka Misri,^h na Wakaldayo waliokuwa wakizingira Yerusalemu wakasikia habari kuhusu. Basi wakaondoka Yerusalemu.ⁱ **6** Kisha neno la Yehova likamjia nabii Yeremia likisema: **7** “Yehova Mungu wa Israeli anasema hivi: ‘Mnapaswa kumwambia hivi mfalme wa Yuda, aliyewatuma kwangu kutafuta habari: ‘Tazama! Jeshi la Farao linalokuja kuwasaidia litalazimika kurudi nchini kwao, Misri.^j **8** Na Wakaldayo watarudi tena na kulishambulia jiji hili na kuliteka na kulitekeza kwa moto.”^k **9** Yehova ana-

37:1 *Pia anaitwa Yehoyakini na Yekonia. #Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

SURA YA 36

a Yer 36:23

SURA YA 37

b 2Fa 24:17-19
1Nya 3:15

c 2Fa 24:12
Yer 22:24

d 2Nya 36:10-12

e Yer 38:1, 4

f 2Fa 25:18, 21
Yer 21:1, 2
Yer 29:25

g Yer 37:15

h Eze 17:15

i Yer 34:21

j Yer 17:5
Omb 4:17
Eze 17:17

k Yer 32:29
Yer 34:22
Yer 39:8

Safu ya 2

a Yer 21:4

b Yer 34:21

c Yer 1:1

d Yer 26:11
Yer 38:4

e Yer 20:2
Ebr 11:32, 36

sema hivi: “Msjidanganye* kwa kusema, ‘Hakika Wakaldayo wataondoka na kutuacha,’ kwa sababu hawataondoka. **10** Hata kama mngeliangamiza jeshi lote la Wakaldayo wanaopigana nanyi na wabaki tu wale waliojeruhiwa, bado wangetoka katika mahema yao na kulitekeza jiji hili kwa moto.””^a

11 Jeshi la Wakaldayo lilipoondoka Yerusalemu kwa sababu ya jeshi la Farao,^b **12** Yeremia akaondoka Yerusalemu na kwenda kwenye nchi ya Benjamini^c ili apate fungu lake huko miongoni mwa watu wake. **13** Lakini alipofika kwenye Lango la Benjamini, ofisa aliyesimamia walenzi, aliyelitwa Iriya mwana wa Shelemia mwana wa Hanania, akamkamata nabii Yeremia na kumwambia: “Unakimbia kwenda kwa Wakaldayo!” **14** Lakini Yeremia akasema: “Si kweli! Mimi sikimbii kwenda kwa Wakaldayo.” Lakini hakumsikiliza. Basi Iriya akamkamata Yeremia na kumpeleka kwa wakuu. **15** Wakuu wakamkasirikia vikali Yeremia,^d nao wakampiga na kumfunga*^e katika nyumba ya mwandishi Yehonathani, iliyo kuwa imefanywa kuwa gereza. **16** Yeremia alitiwa katika gereza lililo chini ya ardhii,^{*} kwenye vyumba vyenye ngo-me, naye akakaa humo kwa siku nyingi.

17 Kisha Mfalme Sedekia akaagiza aletwe, naye mfalme akaanza kumuuliza maswa-

37:9 *Au “msizidanganye nafsi zenu.”
37:15 *Tnn., “wakamtia katika nyumba ya pingu.” 37:16 *Tnn., “nyumba ya tangi.”

li kisiri katika nyumba yake.*^a Akamuuliza, "Je, kuna neno lolote kutoka kwa Yehova?" Yeremia akasema: "Lipo!" naye akaendelea kusema: "Utatiwa mikononi mwa mfalme wa Babiloni!"^b

18 Pia Yeremia akamwambia hivi Mfalme Sedekia: "Nimekutendea dhambi gani wewe na watumishi wako na watu hawa, hivi kwamba mmenifunga gerezani? **19** Wako wapi sasa manabii wenu waliowatabiria kwamba 'Mfalme wa Babiloni hata-kushambulia wewe wala nchi hii'?"^c **20** Sasa sikiliza, tafadhali, ewe bwana wangu mfalme. Tafadhali, kubali ombi langu la kupata kibali. Usinirudishe katika nyumba ya mwandishi Yehonathani,^d la sivyo nitafia humo."^e **21** Basi Mfalme Sedekia akaamuru Yeremia awekwe kifungoni katika Ua wa Walinzi,^f naye alipewa mkate wa mviringo kila siku kutoka kwenye barabara ya waokaji^g mpaka mikate yote ilipokwisha jijini.^h Na Yeremia akaendelea kukaa katika Ua wa Walinzi.

38 Sasa Shefatia mwana wa Matani, Gedalia mwana wa Pashuri, Yukali mwana wa Shelemia, na Pashuri mwana wa Malkiya wakasikia maneno ambayo Yeremia alikuwa akiwaambia watu wote, akisema: **2** "Yehova anasema hivi: 'Yule atakayebaki katika jiji hili atakufa kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari.^k Lakini yule atakayejisalimisha* kwa Wakaldayo atae-

37:17 *Au "jumba lake la mfalme."
38:2 *Tnn., "atakayeenda."

SURA YA 37

a Yer 38:14

b Yer 21:7
Yer 24:8
Yer 34:21
Eze 12:12, 13c Yer 14:13
Yer 23:16, 17
Yer 27:14
Yer 28:1, 2
Omb 2:14

d Yer 37:15

e Yer 26:15
Yer 38:8, 9f Ne 3:25
Yer 32:2
Yer 33:1
Yer 38:13, 28

g 1Fa 17:6

h 2Fa 25:3
Yer 38:9

SURA YA 38

i Yer 37:3

j Yer 21:1, 2

k Yer 27:13
Yer 29:18
Eze 7:15

Safu ya 2

a Yer 21:8-10

b 2Fa 25:1, 2
2Nya 36:17

c Yer 26:11

d Yer 33:1
Yer 37:21
Yer 38:28

e Yer 39:16

f Yer 37:13

ndelea kuishi naye atapata uhai wake* kama nyara" na kuendelea kuishi.^a **3** Yehova anasema hivi: "Kwa kweli jiji hili litatiwa mikononi mwa jeshi la mfalme wa Babiloni, naye ataliteka."^b

4 Wakuu wakamwambia mfalme: "Tafadhali agiza mtu huyu auawe,^c kwa maana hivyo ndivyo anavyoidhoofisha mioyo* ya wanajeshi waliobaki jijini, na pia ya watu wote, kwa kuwaambia maneno hayo. Kwa maana mtu huyu hawata-kii amani watu hawa, bali msiba." **5** Mfalme Sedekia akajibu: "Tazama! Yuko mikononi mwenu, kwa maana mfalme hawezi kufanya jambo lolote ili kuwazuia."

6 Basi wakamchukua Yeremia na kumtupa ndani ya tangi la maji la Malkiya mwana wa mfalme, lililokuwa katika Ua wa Walinzi.^d Wakamshusha Yeremia ndani kwa kamba. Basi hapakuwa na maji ndani ya tangi hilo, ila matope tu, naye Yeremia akaanza kuzama ndani ya matope.

7 Ebed-meleki^e Mwethiopia, towashi* aliyekuwa katika nyumba ya^f mfalme, akasi-kiwa kwamba wamemtia Yeremia ndani ya tangi. Sasa mfalme alikuwa ameketi katika Lango la Benjamini,^f **8** basi Ebed-meleki akatoka katika nyumba ya^f mfalme na kuzungumza na mfalme, akisema: **9** "Ee bwana wangu mfalme, watu hawa wamemtendea Yeremia uovu! Wamemtupa

38:2 *Au "nafsi yake." #Au "atapanyoka na uhai wake."
38:4 *Tnn., "mikonono."
38:7 *Au "ofisa wa makao ya mfalme."
38:7, 8 *Au "jumba la."

ndani ya tangi, naye atafia humo kwa sababu ya njaa kali, kwa maana hakuna mka-te uliobaki jijini.”^a

10 Ndipo mfalme akamwamuru hivi Ebed-meleki Mwe-thiopia: “Chukua watu 30 kutoka mahali hapa, nawe umvute nabii Yeremia kutoka katika tangi hilo kabla hajafa.”

11 Basi Ebed-meleki akawachukua wale watu na kwenda kwenye nyumba ya* mfalme sehemu iliyokuwa chini ya hazina,^b naye akachukua kutoka sehemu hiyo matambara yaliyochakaa na vipande vya nguo vilivyochakaa na kumshushia Yeremia ndani ya tangi hilo kwa kamba. **12** Ndipo Ebed-meleki Mwe-thiopia akamwambia Yeremia: “Tafadhali weka matambara na vipande hivyo vya nguo kati ya makwapa yako na kamba.” Yeremia akafanya hivyo, **13** nao wakamvuta Yeremia nje kwa zile kamba na kumtoa ndani ya tangi hilo. Na Yeremia akaendelea kukaa katika Ua wa Walinzi.^c

14 Mfalme Sedekia akaagiza Yeremia aletwe kwake kwenye mlango wa tatu, ulio katika nyumba ya Yehova, naye mfalme akamwambia Yeremia: “Ningependa kukuuliza jambo fulani. Usinifiche jambo lolote.” **15** Ndipo Yeremia akamwambia Sedekia: “Nikikwambia, kwa kweli utaniau. Nami nikikushauri, hutanisi-kiliza.” **16** Basi Mfalme Sedekia akamwambia Yeremia kisiri, akisema: “Kwa hakika kama Yehova anavyoishi, ambaye ametupatia uhai huu, sitakuua, nami sitakutia miko-

38:11, 22 *Au “jumba la.”

SURA YA 38

a Yer 52:6

b 2Fa 20:13

c Yer 37:21

Safu ya 2

a Yer 21:9

Yer 27:12

b 2Fa 25:8, 9

c 2Fa 25:6

Yer 39:5

d Yer 39:3

e Omb 1:2

noni mwa watu hawa wanaotaka kukuua.”*

17 Kisha Yeremia akamwambia Sedekia: “Yehova, Mungu wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Ukijisalimisha* kwa wakuu wa mfalme wa Babiloni, uhai wako utaokoka,[#] na jiji hili halitaketezwa kwa moto, na wewe na watu wa nyumba yako mtaokoka.’^a **18** Lakini usipojisalimisha* kwa wakuu wa mfalme wa Babiloni, jiji hili litatiwa mikononi mwa Wakaldayo, nao watalitekeza kwa moto,^b nawe hutaponyoka mikononi mwao.”^c

19 Kisha Mfalme Sedekia akamwambia Yeremia: “Ninawaogopa Wayahudi ambao wamekimbia kwenda kwa Wakaldayo, kwa maana nikitiwa mikononi mwao watanitendea ukatili.” **20** Lakini Yeremia akasema: “Hutatiwa mikononi mwao. Tafadhali, itii sauti ya Yehova kuhusiana na yale ninayokuambia, na mambo yatakuendea vema, nawe utaeendelea kuishi. **21** Lakini ukikataa kujisalimisha,* Yehova amenifunulia jambo hili: **22** Tazama! Wanawake wote waliobaki katika nyumba ya* mfalme wa Yuda wanatolewa nje kwa wakuu wa mfalme wa Babiloni,^d nao wanasema,

‘Watu uliowatumaini* wamekudanganya na kukushinda.’^e

Wamefanya mguu wako uzame kwenye matope.

38:16 *Au “wanaotafuta nafsi yako.”

38:17 *Tnn., “ukienda nje.” #Au “nafsi yako itaendelea kuishi.” 38:18 *Tnn., “usipoenda nje.” 38:21 *Tnn., “kwenda nje.” 38:22 #Tnn., “Watu wa amani yako.”

Sasa wamegeuka na kuru-di nyuma.^a

23 Nao wanawatoa nje wake zako wote na wanao wote na kuwapeleka kwa Wakaldayo, nawe hutaponyoka mikononi mwao, lakini utakamatwa na mfalme wa Babiloni,^a na kwa sababu yako, jiji hili litatekezwa kwa moto.”^b

24 Kisha Sedekia akamwambia Yeremia: “Usimwambie mtu yeyote mambo haya, ili usife. **25** Na wakuu wakisia kwamba nimezungumza nawe nao waje na kukuambia, ‘Tafadhali, tuambie ulichomwambia mfalme. Usitufiche jambo lolote, nasi hatutakuua.’^c Mfalme alikuambia nini?’ **26** utawajibu hivi: ‘Nili kuwa niki mwomba mfalme asinirudishe katika nyumba ya Yehonathani ili nisifie humo.’”^d

27 Baadaye wakuu wote wakamjia Yeremia na kumuuliza maswali. Akawaambia mambo yote ambayo mfalme alimwamuru aseme. Basi hakawumwambia jambo lolote zaidi, kwa maana hakuna mtu aliyesikia mazungumzo hayo. **28** Mpaka siku ambayo Yerusalemu lilitekwa, Yeremia alikaa katika Ua wa Walinzi;^e bado alikuwa humo Yerusalemu lilipotekwa.^f

39 Katika mwaka wa tisa wa utawala wa Mfalme Sedekia wa Yuda, katika mwezi wa kumi, Mfalme Nebukadreza* wa Babiloni alikuja Yerusalemu na jeshi lake lote, na kulizingira jiji hilo.^g

2 Katika mwaka wa 11 wa utawala wa Sedekia, mwezi

39:1, 5 * Tnn., “Nebukadreza,” njia nyngine ya kuandika jina hili.

SURA YA 38

a 2Fa 25:7

b Yer 52:8, 13

c Yer 38:4

d Yer 37:15

e Yer 15:20
Yer 32:2
Yer 33:1
Yer 37:21
Yer 39:13, 14

f 2Fa 25:8, 9
2Nya 36:17

SURA YA 39

g 2Fa 25:1, 2
Yer 52:4, 5
Eze 24:1, 2

Safu ya 2

a 2Fa 25:3, 4
Yer 52:6, 7
Eze 33:21

b Yer 1:15

c Kum 28:25

d 2Fa 25:4-7
Yer 52:7-11

e Yer 32:4
Yer 38:18

f 2Fa 23:31, 33

g 2Fa 17:24

h Yer 21:7
Yer 34:18-20

i Eze 12:13

j Isa 5:9
Yer 38:18

k 2Fa 25:9-11
2Nya 36:17, 19
Ne 1:3
Yer 52:13-15

l 2Fa 25:20
Yer 40:1
Yer 52:12

wa nne, siku ya tisa ya mwezi huo, walibomoa sehemu ya ukuta wa jiji.^a **3** Na wakuu wote wa mfalme wa Babiloni wakaingia na kuketi katika Lango la Kati,^b yaani, Nergal-shareza yule Samgari, Nebosarsekimu yule Rabsarisi,* Nergal-shareza yule Rabmagi,[#] na wakuu wengine wote wa mfalme wa Babiloni.

4 Mfalme Sedekia wa Yuda na wanajeshi wote walipowaona walikimbia,^c wakatoa kijini wakati wa usiku kupitia njia ya bustani ya mfalme, kupitia lango lililokuwa kati ya kuta mbili, nao wakuafuata njia inayoelekea Araba.^d

5 Lakini jeshi la Wakaldayo likawafuatia, nao wakamfikia Sedekia katika jangwa tamberare la Yeriko.^e Wakamkamata na kumleta kwa Mfalme Nebukadreza* wa Babiloni kule Ribla^f katika nchi ya Hamathi,^g ambako alimhukumu.

6 Mfalme wa Babiloni akaagiza wana wa Sedekia wachinjwe mbele ya macho yake kule Ribla, na mfalme wa Babiloni akaagiza wakuu wote wa Yuda wachinjwe.^h **7** Ndiipo akayapofusha macho ya Sedekia, kisha akamfunga kwa pingu za shaba ili ampeleke Babiloni.ⁱ

8 Halafu Wakaldayo wakaiteketeza nyumba ya* mfalme na nyumba za watu,^j nao wakazibomoa kabisa kuta za Yerusalemu.^k **9** Nebuzaradani/ mkuu wa walinzi akawapeleka uhamishoni kule Babiloni watu waliobaki jijini, na wale

39:3 * Au kulingana na mpangilio tofauti wa maandishi ya Kiebrania, “Nergal-shareza, Samgari-nebo, Sarsekimu, Rabsarisi.” [#] Au “mchawi mkuu (mnajimu).” **39:8** * Au “jumba la.”

waliojalisimisha kwake, na yote aliyebaki.

10 Lakini Nebuzaradani mkuu wa walinzi aliwaacha katika nchi ya Yuda baadhi ya watu maskini kabisa, wale ambao hawakuwa na chochote. Siku hiyo aliwapatia pia mashamba ya mizabibu na mashamba mengine ili wayalime.*^a

11 Ndipo Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni akamwagiza hivi Nebuzaradani mkuu wa walinzi kumhusu Yeremia: **12** “Mchukue nawe umtunze; usimduru, na umpe chochote atakachokuomba.”^b

13 Basi Nebuzaradani mkuu wa walinzi, Nebushazbani yule Rabsarisi,* Nergal-sharezia yule Rabmagi,[#] na wakuu wote wa mfalme wa Babiloni wakawatuma watu **14** wamtote Yeremia katika Ua wa Walinzi^c na kumkabidhi kwa Gedalia^d mwana wa Ahikamu^e mwana wa Shafani^f ili apeleke nyumbani kwake. Basi akaishi pamoja na watu wengine.

15 Yeremia alipokuwa amefungiwa katika Ua wa Walinzi,^g neno la Yehova lilimjia likisema: **16** “Nenda umwambie Ebed-meleki^h Mwethiopia, ‘Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Ninayatimiza maneno yangu kuhusu jiji hili ili kuleta msiba wala si mema, na siku hiyo utayaona yakitimia.””

17 “Lakini nitakuokoa siku hiyo,’ asema Yehova, ‘nawe

39:10 *Au labda, “wafanye utumishi wa lazima.” **39:11** *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili. **39:13** *Au “ofisa mkuu wa makao ya mfalme.” #Au “mchawi mkuu (mna-jimu).”

SURA YA 39

a 2Fa 25:12
Yer 52:16

b Yer 40:2, 4

c Yer 38:28

d 2Fa 25:22
Yer 40:5
Yer 41:2

e 2Nya 34:20, 21
Yer 26:24

f 2Fa 22:8

g Yer 32:2
Yer 37:21

h Yer 38:7

Safu ya 2

a Yer 45:2, 5

b Zb 37:39, 40
Yer 17:7

SURA YA 40

c Yer 39:9
Yer 52:12, 13

d Yos 18:21, 25

e Yer 50:7

f Yer 39:11, 12

g 2Fa 25:22
Yer 39:13, 14
Yer 41:2

h 2Fa 22:12, 13
Yer 26:24

i 2Fa 22:8

hutatiwa mikononi mwa watu unaowaogopa.’

18 “Kwa maana hakika nitakuokoa, nawe hutakufa kwa upanga. Uhai wako utakuwa* kama nyara,^{#a} kwa sababu ulinitumaini,^b asema Yehova.”

40 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova baada ya Nebuzaradani^c mkuu wa walinzi kumwachilia huru kutoka Rama.^d Alikuwa amepoleka huko akiwa amefungwa pingu mikononi, naye alikuwa miongoni mwa watu wote waliohamishwa kutoka Yerusalemu na Yuda waliokuwa wakipeleka uhamishoni Babiloni. **2** Kisha mkuu wa walinzi akamchukua Yeremia na kumwambia: “Yehova Mungu wako alitabiri msiba huu dhidi ya mahali hapa, **3** na Yehova ameuleta msiba huo kama alivyosema, kwa sababu ninyi watu mlimtendea dhambi Yehova na hamkuitii sauti yake. Ndiyo sababu jambo hili limewapata.^e **4** Sasa ninakufungua pingu zilizo mikononi mwako. Ikiwa unaona ni vema kwako kwenda pamoja nami Babiloni, njoo, nami nitakutunza. Lakini ikiwa hutaki kwenda pamoja nami Babiloni, usije. Angalia! Nchi nzima iko mbele yako. Nenda popote unapotaka.”^f

5 Hata kabla Yeremia haja-geuka kuondoka, Nebuzaradani akamwambia: “Rudi kwa Gedalia^g mwana wa Ahikamu^h mwana wa Shafani,ⁱ ambaye mfalme wa Babiloni amemweka juu ya majiji ya Yuda, nawe ukae pamoja naye miongoni mwa watu; au uende popote unapotaka.”

39:18 *Au “nafsi yako itakuwa.” #Au “Utaponyoka na uhai wako.”

Ndipo mkuu wa walenzi aka-mpa posho ya chakula na zawadi, akamruhusu aende zake. **6** Basi Yere-mia akae-nda kwa Gedalia mwana wa Ahikamu kule Mispa^a na kukaa pamoja naye miongoni mwa watu waliobaki nchini.

7 Baadaye wakuu wote wa majeshi waliokuwa uwanjani pamoja na watu wao wakasi-kiya kwamba mfalme wa Babi-loni amemweka Gedalia mwana wa Ahikamu awe msimami-zi wa nchi na kwamba aliku-wa amemweka awe msimamizi wa wanaume, wanawake, na watoto, watu maskini nchi-ni ambao hawakuwa wamepe-lekwa uhamishoni Babiloni.^b

8 Basi wakaenda kwa Geda-lia huko Mispa.^c Wakuu hao ni Ishmaeli^d mwana wa Nethania, Yohanani^e na Yonathani wana wa Karea, Seraya mwana wa Tanhumethi, wana wa Efa-i Mnetofa, na Yezania^f mwana wa Mmaakathi, pamoja na wanajeshi wao. **9** Geda-lia mwana wa Ahikamu mwana wa Shafani akawaapia wao pamoja na wanajeshi wao, aki-sema: "Msiogope kuwatumi-kiya Wakaldayo. Kaeni katika nchi hii na kumtumikia mfal-me wa Babiloni, na mambo ya-tawaenda vema."^g **10** Lakini mimi, nitakaa Mispa, ili niwa-wakilishe kwa* Wakaldayo wa-takaokuja kwetu. Lakini ninyi mnapaswa kukusanya divai, matunda ya wakati wa kianga-zi, na mafuta na kuviweka vitu hivyo katika vyombo vyenu vya kuhifadhia na mkae kati-ka majiji mliyoyachukua."^h

11 Na Wayahudi wote walio-kuwa Moabu, Amoni, na Edo-

40:10 *Tnn., "nisimame mbele ya."

SURA YA 40

a Amu 20:1
1Fa 15:22

b 2Fa 25:22
Yer 39:10

c 2Fa 25:23

d 2Fa 25:25

e Yer 41:11, 16
Yer 43:2

f Yer 42:1, 2

g 2Fa 25:24
Yer 27:11

h Yer 39:10

Safu ya 2

a Yer 41:10

b Yer 41:2

c 2Fa 25:22

SURA YA 41

d 2Fa 25:23
Yer 40:14

mu, na wale waliokuwa kati-ka nchi nyingine zote, waka-sikia pia kwamba mfalme wa Babiloni alikuwa amewaa-cha watu fulani wabaki Yuda na kwamba alikuwa amemwe-ka Gedalia mwana wa Ahika-mu mwana wa Shafani awe msimamizi wao. **12** Basi Wa-yahudi wote wakaanza kuru-di kutoka kila mahali ambako walikuwa wametawanywa, nao wakaja katika nchi ya Yuda, kwa Gedalia huko Mispa. Nao wakakusanya divai na matunda ya wakati wa kianga-zi kwa wingi sana.

13 Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi waliokuwa uwanjani wa-kaja kwa Gedalia huko Mispa. **14** Wakamwambia: "Je, hujui kwamba Baalisi mfal-me wa Waamoni,^a amemtu-ma Ishmaeli mwana wa Ne-thania akuue?"^{*b} Lakini Geda-lia mwana wa Ahikamu haku-waamini.

15 Kisha Yohanani mwana wa Karea akamwambia kisi-ri Gedalia huko Mispa: "Ni-nataka kwenda kumua Ishmaeli mwana wa Nethania, na hakuna mtu atakaye-jua. Kwa nini akuue,^{*} na kwa nini watu wote wa Yuda waliokusanyika kwako watawa-nyike na watu wa Yuda walio-baki waangamie?" **16** Lakini Gedalia^c mwana wa Ahikamu akamwambia Yohanani mwana wa Karea: "Usifanye hivyo, kwa maana unasema uwongo kumhusu Ishmaeli."

41 Katika mwezi wa saba, Ishmaeli^d mwana wa Ne-thania mwana wa Elishama, aliyekuwa wa uzao wa

40:14, 15 *Au "aiue nafsi yako."

kifalme* na mmoja kati ya wakuu wa mfalme, akaja pamoja na wanaume wengine kumi kwa Gedalia mwana wa Ahikamu huko Mispa.^a Walipokuwa wakila chakula pamoja huko Mispa, **2** Ishmaeli mwana wa Nethania na wale watu kumi waliokuwa pamoja naye wakasimama na kumpiga kwa upanga Gedalia mwana wa Ahikamu mwana wa Shafani. Kwa hiyo akamuua mtu ambaye mfalme wa Babiloni alikuwa amemweka kuwa msimamizi nchini. **3** Ishmaeli aliwaua pia Wayahudi wote waliokuwa pamoja na Gedalia huko Mispa, na pia wanajeshi Wakaldayo waliokuwa huko.

4 Siku ya pili baada ya Gedalia kuuawa, kabla mtu yeyote hajajua jambo hilo, **5** wakaja watu 80 kutoka Shekemu,^b kutoka Shilo,^c na kutoka Samaria.^d Ndevu zao zilikuwa zimenyolewa, mavazi yao yalikuwa yameraruka, walikuwa wamejikatakata,^e nao walikuwa na matoleo ya nafaka na uvumba^f mikononi mwao ili wavilete vitu hivyo katika nyumba ya Yehova. **6** Basi Ishmaeli mwana wa Nethania akatoka Mispa ili kuwapokea, naye alikuwa akitembea huku akilia. Alipokutana nao, akawaambia: "Njooi kwa Gedalia mwana wa Ahikamu." **7** Lakini walipoingia jijini, Ishmaeli mwana wa Nethania na watu wake wakawachinja na kuwatupa ndani ya tangi la maji.

8 Lakini kulikuwa na watu kumi kati yao waliomwambia Ishmaeli: "Usituue, kwa maana shambani tuna maghala

SURA YA 41

a 2Fa 25:25

b 1Fa 12:1

c Yos 18:1

d 1Fa 16:23, 24

e Law 19:27, 28
Kum 14:1

f Law 2:1

Safu ya 2

a 1Fa 15:22
2Nya 16:6

b Yer 40:12

c Yer 40:7

d Yer 40:14

e Yer 40:13
Yer 43:2

f Yer 40:6

yaliyofichwa ya ngano, shayiri, mafuta, na asali." Basi hakuwaua pamoja na ndugu zao. **9** Sasa Ishmaeli akazitupa maiti zote za watu alio waua ndani ya tangi kubwa la maji, tangi ambalo Mfalme Asa alitengeneza kwa sababu ya Mfalme Baasha wa Israeli.^a Hilo ndilo tangi ambalo Ishmaeli mwana wa Nethania alilijaza maiti za watu waliouawa.

10 Ishmaeli akawachukua mateka watu wote waliobaki huko Mispa,^b kutia ndani mabinti wa mfalme na watu wote waliobaki Mispa, ambao Nebuzaradani mkuu wa walenzi alikuwa amewaweka chini ya ulinzi wa Gedalia^c mwana wa Ahikamu. Ishmaeli mwana wa Nethania aliwachukua mateka na kuvuka kwenda kwa Waamoni.^d

11 Yohanani^e mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi waliokuwa pamoja naye waliposikia uovu wote ambao Ishmaeli mwana wa Nethania alikuwa ametenda, **12** wakawachukua wanaume wote na kwenda kupigana na Ishmaeli mwana wa Nethania, nao wakamkuta kando ya maji mengi* kule Gibeoni.

13 Watu wote waliokuwa pamoja na Ishmaeli wakashingilia walipomwona Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi waliokuwa pamoja naye. **14** Ndipo watu wote ambao Ishmaeli alikuwa amewachukua mateka kutoka Mispa^f wakageuka na kurudi pamoja na Yohanani mwana wa Karea. **15** Lakini Ishmaeli mwana wa Nethania

41:12 *Au labda, "dimbwi kubwa."

41:1 *Tnn., "wa mbegu ya ufalme."

pamoja na wanaume wanane kati ya watu wake wakamtoroka Yohanani, na kwenda kwa Waamoni.

16 Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi waliokuwa pamoja naye wakawachukua watu waliobaki Mispa ambao walikuwa wamewaokoa kutoka kwa Ishmaeli mwana wa Nethania baada ya kumuua Gedalia^a mwana wa Ahikamu. Wakawaleta wanaume, wanajeshi, wanawaake, watoto, na maofisa wa makao ya mfalme kutoka Gibeoni. **17** Basi wakaenda na kuka mahali pa kulala pa Kimhamu kando ya Bethlehemu,^b wakikusudia kwenda Misri,^c **18** kwa sababu ya Wakaldayo. Kwa maana waliwaogopa, kwa sababu Ishmaeli mwana wa Nethania alikuwa amemuua Gedalia mwana wa Ahikamu, ambaye mfalme wa Babiloni alikuwa amemweka kuwa msimamizi wa nchi.^d

42 Kisha wakuu wote wa jeshi, na Yohanani^e mwana wa Karea, Yezania mwana wa Hoshaya, na watu wote, kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi, wakaribia **2** na kumwambia nabii Yeremia: “Tafadhali, sikia ombi letu la kutaka kibali nawe usali kwa ajili yetu kwa Yehova Mungu wako, kwa ajili ya watu hawa wote waliobaki, kwa maana kati ya watu wengi, wachache ndio waliobaki,^f kama unavyoona. **3** Yehova Mungu wako na atua mbie njia tunayopaswa kufuata na jambo tunalopaswa kufanya.”

4 Nabii Yeremia akawajibu: “Nimewasikia, nami ninasali kwa Yehova Mungu wenu ku-

SURA YA 41

a Yer 41:2

b Mwia 35:19

c 2Fa 25:26
Yer 42:14
Yer 43:7

d Yer 41:2

SURA YA 42

e Yer 40:13, 14

f Kum 28:62

Safu ya 2

a Yer 41:16

b Kum 32:36
Yer 18:7, 8
Mik 7:18

c Yer 41:17, 18

d Kut 34:6

lingana na ombi lenu; na kila neno ambalo Yehova atawajibu, nitawaambia. Sitawaficha neno lolote.”

5 Wakamjibu Yeremia: “Yehova na awe shahidi wa kweli na mwaminifu dhidi yetu ikiwa hatutafanya sawasawa kama anavyotuagiza Yehova Mungu wako kupitia wewe.

6 Iwe ni jambo jema au baya, tutaitii sauti ya Yehova Mungu wetu ambaye tunakutuma kwake, ili mambo yatuendee vema kwa sababu tunaitii sauti ya Yehova Mungu wetu.”

7 Baada ya siku kumi neno la Yehova likamjia Yeremia.

8 Basi akamwita Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi waliokuwa pamoja naye na watu wote, kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi.^a **9** Akawaambia: “Yehova Mungu wa Israeli, ambaye mlinituma kwake ili kupeleka ombi lenu la kutaka kibali mbele zake, anasema hivi: **10** ‘Ikiwa kwa kweli mtakaa katika nchi hii, basi nitawajenga nami sitawabomoa, nitawapanda nami sitawang’oa, kwa maana nitaghairi* kuhusu msiba ambao nimewaletea.^b **11** Msimwogope mfalme wa Babiloni, mnyamwogopa.’^c

“Msimwogope,” asema Yehova, ‘kwa maana niko pamoja nanyi, ili kuwaokoa na kuwakomboa kutoka mikononi mwake. **12** Nami nitawoonyesha rehema,^d naye atawoonyesha rehema na kuwarudisha kwenye nchi yenu wenyewe.

13 “‘Lakini mkisema, ‘Hapana, hatutakaa katika nchi

42:10 *Au “nitahuzunika.”

hii!” nanyi mkose kuitii sauti ya Yehova Mungu wenu **14** kwa kusema: “Hapana, badala yake tutaenda katika nchi ya Misri,^a ambako hatutaona vita wala kusikia sauti ya peembe wala kuwa na njaa kwa kukosa mkate; huko ndiko tutakakoishi,” **15** basi sikieni neno la Yehova, enyi watu wa Yuda mliobaki. Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: “Ikiwa mmeazimia kabisa kwenda Misri nanyi mwende kukaa huko,* **16** ndipo upanga ulleule ambao mnaogopa utawafikia huko katika nchi ya Misri, na njaa ileile ambayo mnaogopa itawafuata huko Misri, nanyi mtafia huko.^b **17** Na watu wote walioazimia kwenda Misri ili kukaa huko watakufa kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari. Hakuna yeyote kati yao atakayeokoka au kuponyoka msiba nitakaowaletea.”

18 “Kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Kama hasira yangu na ghadhabu yangu ilivyomwagwa juu ya wakaaji wa Yerusalemu,^c ndivyo ghadhabu yangu itakavyomwagwa juu yenu ikiwa mtaenda Misri, nanyi mtakuwa laana, kitu cha kutisha, matusi, na shutuma,^d nanyi hamtapaona tena kamwe mahali hapa.’

19 “Yehova amewakataza, enyi watu wa Yuda mliobaki. Msiende Misri. Mnapaswa kujua kwa hakika kwamba nimewaonya leo, **20** kwamba kosa lenu litawagharimu uhai wenu.* Kwa maana mlinitu-

42:15 *Au “mwende kukaa huko kwa muda.” 42:20 *Au “nafsi zenu.”

SURA YA 42

a Yer 43:4, 7

b Kum 28:45
Yer 44:12-14
Yer 44:27, 28c 2Fa 25:8-10
2Nya 34:24, 25
2Nya 36:16, 17
Omb 2:4

d Yer 29:18

Safu ya 2

a Yer 42:1, 2

b 2Nya 24:19
Ne 9:26
Zek 7:11

c Yer 43:10, 11

SURA YA 43

d Yer 41:16
Yer 42:1-3e Yer 36:4
Yer 45:1

f Yer 38:4, 6

g Yer 40:11, 12

ma kwa Yehova Mungu wenu, mkisema, ‘Sali kwa ajili yetu kwa Yehova Mungu wetu, nawe utuambie kila jambo ambalo Yehova Mungu wetu anasema, nasi tatalifanya.’^a **21** Nami nimewaambia leo, lakini hamtaitii sauti ya Yehova Mungu wenu wala kufanya jambo lolote alilonituma niwaambie.^b **22** Kwa hiyo, jueni kwa haka kwamba mtakufa kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari mahali mnapotamani kwenda kuishi.”^c

43 Yeremia alipomaliza kuwaambia watu wote maneno hayo yote kutoka kwa Yehova Mungu wao, kila neno ambalo Yehova Mungu wao alikuwa amemtuma awaambie, **2** Azaria mwana wa Hoshaya, Yohanani^d mwana wa Karea, na watu wote wenye kimbelebele wakamwambia Yeremia: “Unasema uwongo! Yehova Mungu wetu hakukutuma useme, ‘Msiende kukaa Misri.’ **3** Lakini Baruku^e mwana wa Neria anakuchochea dhidi yetu ili kututia mikononi mwa Wakaldayo, ili watuue au kutupeleka uhamishoni Babiloni.”^f

4 Basi Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi na watu wote hawakuitii sauti ya Yehova kwamba wabaki katika nchi ya Yuda. **5** Badala yake, Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa jeshi wakawachukua watu wote wa Yuda waliobaki ambao walikuwa wamerudi kuishi katika nchi ya Yuda kutoka katika mataifa yote ambako walikuwa wametawanywa.^g **6** Wakawachukua wanaume, wanawake, wa-

toto, mabinti wa mfalme, na kila mtu ambaye Nebuzaradani^a mkuu wa walinzi alikuwa amemwacha pamoja na Gedalia^b mwana wa Ahikamu^c mwana wa Shafani,^d na pia nabii Yeremia na Baruku mwana wa Neria. **7** Nao wakaingia nchini Misri, kwa maana hawakuitii sauti ya Yehova, wakaenda mpaka Tahpanhesi.^e

8 Kisha neno la Yehova likamjia Yeremia huko Tahpanhesi likisema: **9** "Beba mkononi mwako mawe makubwa, nawe uyafiche katika saruji kwenye ngazi ya matofali iliyo kwenye mlango wa nyumba ya Farao huko Tahpanhesi, huku wanaume Wayahudi wakitazama. **10** Kisha uwaambie, 'Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: "Tazameni, ninamwita Nebukadreza* mfalme wa Babiloni, mtumishi wangu,^f nami nitakiweka kiti chake cha ufalme juu ya mawe haya ambayo nimeyaficha, naye atalitandaza hema lake la kifalme juu yake.^g **11** Naye ataingia na kuipiga nchi ya Misri.^h Yeyote aliyekusudiwa kufa kwa ugonjwa hatari atakufa kwa ugonjwa hatari, na yeyote aliyekusudiwa kwenda utekwani ataenda utekwani, na yeyote aliyekusudiwa kufa kwa upanga atakufa kwa upanga.ⁱ **12** Nami nitaziwasha moto nyumba za* miungu ya Misri,^j naye ataitekeza na kuchiukua mateka. Atajifunika kwa nchi ya Misri kama mchunjaji anavyojifunika kwa vazi lake, naye ataondoka huko

43:10 *Tnn., "Nebukadreza," njia nyngine ya kuandika jina hili. **43:12** *Au "atayawasha moto mahkalu ya."

SURA YA 43

a Yer 39:10

b 2Fa 25:22

c 2Nya 34:20, 21
Yer 26:24

d 2Fa 22:8

e Yer 2:14, 16
Yer 44:1
Eze 30:4, 18f Yer 25:9
Yer 27:6
Eze 29:19, 20g Da 2:21
Da 5:18h Yer 25:17, 19
Yer 46:13
Eze 29:19
Eze 30:4, 18i Yer 44:13
Eze 5:12

j Yer 46:25

Safu ya 2

SURA YA 44

a Yer 43:4, 7

b Eze 29:10
Eze 30:6

c Eze 30:18

d Yer 46:14
Eze 30:16e Eze 29:14
Eze 30:14f 2Fa 25:9, 10
Yer 39:8

g Omb 1:1

h Yer 11:17

i Kum 13:6-9
Kum 32:17
Yer 19:4j 2Nya 36:15, 16
Isa 65:2
Yer 7:24-26
Yer 35:15

k Yer 19:13

l Isa 6:11
Yer 39:8

kwa amani.* **13** Naye atazi-vunja vipandevipande nguzo za* Beth-shemeshi[#] katika nchi ya Misri, naye atazitekeza kwa moto nyumba za^Δ miungu ya Misri."'''

44 Neno lililomjia Yeremia kwa ajili ya Wayahudi wote waliokuwa wakiishi katika nchi ya Misri,^a wale waliokuwa wakiishi Migdoli,^b Tahpanhesi,^c Nofu,[#] ^d na katika nchi ya Pathrosi,^e likisema: **2** "Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: 'Mmeona msiba wote nilioleta dhidi ya Yerusalemu^f na dhidi ya majiji yote ya Yuda, na leo yamebaki magofu, bila mkaaji.^g **3** Ni kwa sababu ya mambo maovu waliyofanya ili kunikasirisha kwa kwenda kutoa dhabihu^h na kuiabudu miungu mingine ambayo hawakujua, wala ninyi wala mababu zenu.ⁱ **4** Niliendelea kuwatuma kwenu watumishi wangu wote manabii, niliwatuma tena na tena* nikisema: "Tafadhali msifanye jambo hili lenye kuchukiza ninalochukia."^j **5** Lakini hawakusikiliza wala kutegea sikio lao na kuacha uovu wao na kuacha kuitolea dhabihu miungu mingine.^k **6** Basi ghadhabu yangu na hasira yangu ilimwagwa na kuwaka katika majiji ya Yuda na kwenye barabara za Yerusalemu, na majiji hayo yakawa magofu na ukiwa, kama ilivyo leo.^l

7 "Na sasa Yehova, Mungu wa majeshi, Mungu wa

43:12 *Au "bila madhara." **43:13** *Au "minara ya." [#]Au "Nyumba (Hekalu la) ya Jua," yaani, Heliopolisi. ^ΔAu "mahkalu ya." **44:1** *Au "Memfsi." **44:4** *Tnn., "nikiamka mapema na kuwatumu."

Israeli, anasema hivi: ‘Kwa nini mnajiletea msiba mku-bwa, ili kila mwanamume na mwanamke, mtoto mdogo na mtoto anayenyonya, waangamie kutoka Yuda, asibaki yeyote? **8** Kwa nini mnikasirisheshe kwa kazi za mikono yenu kwa kuitolea dhabihu miungu mingine katika nchi ya Misri, ambako mmeenda kukaa? Mtaangamia na kuwa kitu cha kulaaniwa na shutuma miongoni mwa mataifa yote ya dunia.^a **9** Je, mmeyasahau matendo maovu ya mababu zenu na matendo maovu ya wafalme wa Yuda^b na matendo maovu ya wake zao,^c na pia matendo yenu maovu na matendo maovu ya wake zenu,^d yaliyofanywa katika nchi ya Yuda na kwenye barabara za Yerusalemu? **10** Mpaka leo hii hawajajinyenyekeza,* hawajaogopa,^e wala hawajafuata sheria yangu na amri zangu nilizoweke mbele yenu na mbele ya mababu zenu.’^f

11 “Kwa hiyo Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Tazameni, nimeazimia kuwaletea msiba, kuiangamiza nchi yote ya Yuda. **12** Nami nitawachukua watu wa Yuda waliobaki walioazimia kwenda nchini Misri kukaa huko, na wote wataangamia nchini Misri.^g Watauawa kwa upanga na kuangamia kwa njaa kali; kuanzia mdogo zaidi mpaka mku-bwa zaidi, watakufa kwa upanga na kwa njaa kali. Nao watakuwa laana, kitu cha kutisha, matusi, na shutuma.^h **13** Nitawaadhibu wale wanaoishi nchini Misri kama nili-

44:10 *Au “hawajahisi wamepondeka.”

SURA YA 44

a 1Fa 9:7
Yer 24:9
Yer 42:18

b 2Fa 21:19, 20
2Fa 24:8, 9

c 1Fa 11:1-3

d Yer 44:19

e Yer 36:22-24

f Kum 6:1, 2

g Eze 30:13

h Yer 42:17, 18

Safu ya 2

a Yer 21:9
Yer 42:22
Yer 43:11

b Yer 43:4, 7

c Yer 44:1

d Yer 7:18

vyoliadhibu Yerusalemu, kwa upanga, kwa njaa kali, na kwa ugonjwa hatari.^a **14** Na watu wa Yuda waliobaki ambao wameenda kukaa nchini Misri hawataponyoka wala kuokoka na kurudi kwenye nchi ya Yuda. Watatamani kurudi na kukaa huko, lakini hawatarudi, isipokuwa wachache watakaoponyoka.”

15 Wanaume wote waliojua kwamba wake zao waliokuwa wakiitolea miungu mingine dhabihu na wake wote waliokuwa wamesimama hapo, wakiwa kundi kubwa, na watu wote waliokuwa wakiishi nchini Misri,^b kule Palthrosi,^c wakamjibu hivi Yermia: **16** “Hatutasikiliza neno ulilotuambia katika jina la Yehova. **17** Badala yake, hakika tutafanya kila neno ambalo vinywa vyetu vimesema, tutamtolea dhabihu Malkia wa Mbinguni* na kumminia matoleo ya kinywaji,^d kama vile sisi, mababu zetu, wafalme wetu, na wakuu wetu walivyofanya katika majiji ya Yuda na kwenye barabara za Yerusalemu tulipokuwa tumeshiba mkate na tulipokuwa na hali njema, wakati ambapo hatukuona msiba wowote. **18** Tangu tulipoacha kumtolea dhabihu Malkia wa Mbinguni* na kumminia matoleo ya kinywaji, tumekosa kila kitu nasi tumeangamia kwa upanga na kwa njaa kali.”

19 Wanawake wakasema: “Na tulipokuwa tukimtolea dhabihu Malkia wa Mbinguni* na kumminia matoleo ya ki-

44:17-19 *Jina la mungu wa kike aliyeabudiwa na Waisraeli waasi imani; hue-nda ni mungu wa kike wa uzazi.

nywaji, je, tulitengeneza keki za dhahihu zinazofanana naye na kummiminia matoleo ya kinywaji bila idhini ya waume zetu?"

20 Kisha Yeremia akawaambia hivi watu wote, wanauame na wake zao na watu wote waliokuwa wakizungumza naye: **21** "Dhahihu ambazo ninyi, mababu zenu, wafalme wenu, wakuu wenu, na watu wa nchi walitoa katika majiji ya Yuda na kwenye barabara za Yerusalemu^a—Yehova alizikumbuka nazo zikaingia moyoni mwake! **22** Mwishowe Yehova hangeweza tena kuvumilia matendo yenu maovu na mambo yenye kuchukiza mliyokuwa mmefanya, nayo nchi yenu ikawa ukiwa, kitu cha kutisha na laana, bila mkaaji, kama ilivyo leo.^b **23** Ni kwa sababu mmetoa dhahihu hizi na kwa sababu mmentendea dhambi Yehova, kwa kutotii sauti ya Yehova na kutofuata sheria yake, amri zake, na vikumbusho vyake, ndiyo sababu msiba huu umewapata, kama ilivyo leo."^c

24 Yeremia akaendelea kuwaambia hivi watu wote na wanawake wote: "Sikieni neno la Yehova, ninyi nyote watu wa Yuda mlio nchini Misri. **25** Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: 'Mambo ambayo ninyi na wake zenu mmesema kwa vinywa vyenu, mmeyatimiza kwa mikonono yenu, kwa maana mlisema: "Hakika tutatimiza nadhiri zetu za kumtolea dhahihu Malkia wa Mbinguni* na ku-

44:25 * Jina la mungu wa kike aliyeabudiwa na Waisraeli waasi imani; huenda ni mungu wa kike wa uzazi.

SURA YA 44

a Yer 11:13
Eze 16:24, 25

b 1Fa 9:8, 9
Omb 2:15
Eze 33:29

c 2Nya 36:15, 16
Da 9:11

Safu ya 2

a Yer 7:18
Yer 44:15, 17

b Eze 20:39

c Isa 48:1, 2
Yer 5:2

d Yer 1:10

e Yer 44:12

f Law 26:44
Isa 27:13
Yer 44:14

g 2Fa 25:7
Yer 34:21
Yer 39:5

mminia matoleo ya kinywaji."^a Hakika ninyi wanawake mtatekeleza nadhiri zenu na kuzitimiza nadhiri zenu.'

26 "Kwa hiyo sikieni neno la Yehova, ninyi nyote watu wa Yuda mnaoishi nchini Misri: "Ninaapa kwa jina langu mwenyewe lililo kuu," asema Yehova, "kwamba jina langu halitatajwa tena katika kiapo na mtu yeyote wa Yuda^b katika nchi yote ya Misri anayesema, 'Kwa hakika kama anavyoishi Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova!'^c **27** Sasa ninawatazama ili kuwaletea msiba bali si mema;^d watu wote wa Yuda walio nchini Misri wataangamia kwa upanga na kwa njaa kali, mpaka watakapokwisha kabisa.^e **28** Ni wachache tu watakaoponyoka upanga nchini Misri na kurudi katika nchi ya Yuda.^f Kisha watu wote wa Yuda waliobaki ambao walienda kuka nchini Misri watajua ni neno la nani lililotimia, langu au lao!"^g

29 "'Na hii ndiyo ishara kwenu,' asema Yehova, 'kwamba nitawaadhibu mahali hapa, ili mjue kwamba maneno niliyosema kuhusu kuwaletea msiba hakika yatatimia. **30** Yehova anasema hivi: "Ninamtia Farao Hofra, mfalme wa Misri, mikononi mwa maa-dui wake na wale wanaotaka kumuua,* kama nilivyomtia Mfalme Sedekia wa Yuda mikononi mwa Mfalme Nebukadredza[#] wa Babiloni, aliyekuwa adui yake na ambaye alitaka kumuua."^g

44:30 * Au "wanaoitafuta nafsi yake."[#] Tnn., "Nebukadredza," njia nyingine ya kuandika jina hili.

45 Hili ndilo neno ambalo nabii Yeremia alimwambia Baruku^a mwana wa Neria alipoandika katika kitabu maneno haya aliyoaambiwa na Yeremia^b katika mwaka wa nne wa utawala wa Yehoyakimu^c mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda:

2 “Yehova Mungu wa Israel anasema hivi kukuhusu wewe, Baruku, **3** ‘Umesema: “Ole wangu, kwa maana Yehova ameongeza huzuni kwenye maumivu yangu! Nimechoka kwa sababu ya kulia kwa maumivu, nami sijapata mahali pa kupumzika.”

4 “Mwambie, ‘Yehova anasema hivi: “Tazama! Kile ambacho nimekijenga nina-kibomoa, na kile nilichokipanda ninaking’oa—nchi yote.^d

5 Lakini unajitafutia* mambo makuu. Acha kuyatafuta mambo hayo.”

“Kwa maana, niko karibu kuleta msiba dhidi ya wote wenye mwili,^{#e} asema Yehova, ‘na popote utakapoenda, nitakupa uhai wako^Δ kuwa nyara.’”^{¶f}

46 Hili ndilo neno la Yehova kwa nabii Yeremia kuhusu mataifa:^g **2** Kuhusu Misri,^h kuhusu jeshi la Farao Nekoⁱ mfalme wa Misri, aliye-kuwa kando ya Mto Efrati na aliyeshindwa huko Karkemishi na Mfalme Nebukadnaza* wa Babiloni katika mwaka wa nne wa utawala wa Yehoyakimu^c mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda:

45:5 *Au “unatarajia.” #Au “watu wote.” ΔAu “nafsi yako.” ¶Au “nitaa-cha uponyoke na uhai wako.” **46:2** *Tnn., “Nebukadnaza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

SURA YA 45

a Yer 32:12
Yer 43:3

b Yer 36:4, 32

c Yer 25:1
Yer 36:1

d Isa 5:5
Yer 1:1, 10

e Isa 66:16
Yer 25:17, 26
Sef 3:8

f Yer 21:9
Yer 39:18
Yer 43:6

SURA YA 46

g Yer 1:10

h Yer 25:15, 19
Eze 29:2
Eze 32:2

i 2Nya 35:20

j 2Fa 23:36
Yer 25:1
Yer 36:1

Safu ya 2

a 2Fa 24:7

b Eze 29:3
Eze 32:2

3 “Tayarisheni ngao ndogo* na ngao kubwa, Na mwende kupigana.

4 Wafungeni farasi lijamu na mpande juu yake, enyi wapanda farasi. Shikeni nafasi zenu na mvae kofia zenu. Sugueni mikuki na mvae makoti yenu ya vita.

5 ‘Kwa nini ninawaona wame-shikwa na hofu? Wanarudi nyuma, mashujaa wao wamepondwa-pondwa. Wamekimbia kwa woga, mashujaa wao hawaku-geuka. Kuna hofu kila mahali,’ asema Yehova.

6 ‘Wenye mbio hawawezi kukimbia, na mashujaa hawawezi kuponyoka.

Kule kaskazini, kwenye ukingo wa Mto Efrati, Wamejikwaa na kuan-guka.’^a

7 Ni nani huyu anayepanda kama Mto Nile, Kama mito iliyofurika maji?

8 Misri inakuja kama Mto Nile,^b Kama mito iliyofurika maji,

Nayo inasema, ‘Nitapanda na kuifunika dunia.

Nitaliangamiza jiji na wale wanaokaa humo.’

9 Pandeni, enyi farasi! Nendeni kiwazimu, enyi magari!

Acheni mashujaa wasonge mbele,

46:3 *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale.

Kushi na Putu, wanaobeba ngao.^a

Na Ludimu,^b wanaobeba na kuupinda* upinde.^c

10 "Siku hiyo ni ya Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, siku ya kisasi ya kulipiza kisasi dhidi ya maadui wake. Na upanga utanyafua na kujishibisha na kunywa damu yao mpaka ushibe, kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, ana dhabihu* katika nchi ya kaskazini kando ya Mto Efrati.^d

11 Panda mpaka Gileadi uchukue zeri.^e

Ewe bikira, binti ya Misri. Umezidisha matibabu yako bure tu,

Kwa maana hakuna tiba kwa ajili yako.^f

12 Mataifa yamesikia kuhusu aibu yako,^g

Na kilio chako kimejaa nchini.

Kwa maana shujaa anajikwaa juu ya shujaa,

Na wote wawili wanaanguka pamoja.^h

13 Hili ndilo neno ambalo Yehova alimwambia nabii Yeremia kuhusu kuja kwa Mfalme Nebukadnaza* wa Babiloni kuishambulia nchi ya Misri.ⁱ

14 "Lisemeni katika Misri, litangazeni huko Migdoli.^j Litangazeni huko Nofu* na Tahpanhesi.^k

Semeni, 'Shikeni nafasi zenu na mjitayarisha,

SURA YA 46

a Eze 27:2, 10

b Mwa 10:6, 13
Eze 30:4, 5

c Isa 66:19

d 2Fa 24:7

e Mwa 37:25
Yer 8:22

f Eze 30:21

g Eze 32:9

h Yer 43:10
Eze 29:19
Eze 30:10

i Yer 44:1
Eze 29:10
Eze 30:6

j Yer 43:4, 7
Eze 30:18

Safu ya 2

a Eze 29:3

b Yos 19:17, 22
Amu 4:6
Zb 89:12

c 1Fa 18:42

d Eze 32:15

Kwa maana upanga utanyafua pande zote kuwazunguka.

15 Kwa nini watu wako wenye nguvu wamefagiliwa mbali?

Walishindwa kusimama imara,

Kwa maana Yehova amewasukuma na kuwaangusha chini.

16 Wanajikwaa na kuanguka kwa wingi.

Wanaambiana:

"Inukeni! Acheni turudi kwa watu wetu na kwenye nchi yetu

Kwa sababu ya upanga ulio katili."

17 Huko wametangaza, 'Farao mfalme wa Misri ni kelele isiyu na maana Ambaye ameacha nafasi impite.'^{*a}

18 'Kwa hakika kama nina-vyoishi,' asema Mfalme, ambaye jina lake ni Yehova wa majeshi,

'Ataingia* kama Tabori^b kati ya milima

Na kama Karmeli^c kando ya bahari.

19 Tayarisha mzigo wako kwa ajili ya uhamisho, Ewe binti unayekaa Misri. Kwa maana Nofu* itakuwa kitu cha kutisha; Itawashwa moto^d na kucha bila mkaaji.^d

20 Misri ni kama ndama jike anayependeza, Lakini wadudu wanaouma watamvamia kutoka kaskazini.

46:17 *Tnn., "wakati uliowekwa umpite." **46:18** *Yaani, yule atakayeishinda Misri. **46:19** #Au labda, "Itakuwa mahame."

46:9 *Tnn., "kuukanyaga." **46:10** *Au "mauaji." **46:13** *Tnn., "Nebukadnaza," njia nyingine ya kuandika jina hili. **46:14, 19** #Au "Memfisi."

21 Hata wanajeshi wake waliokodiwa walio kati yake ni kama ndama waliononeshwa,

Lakini wao pia wamegeuka na kukimbia pamoja.

Walishindwa kusimama imara,^a

Kwa maana siku yao ya msiba imewajia,

Wakati wao wa kuadhibiwa.*

22 ‘Sauti yake ni kama ya nyoka anayenyiririka, Kwa maana wanamfuata kwa nguvu, wakiwa na mashoka,

Kama wanaume wanaokata miti.*

23 Wataukata msitu wake,’ asema Yehova, ‘ingawa ulionekana hauwezi kupenywa.

Kwa maana ni wengi sana kuliko nzige, nao hawahesabiki.

24 Hakika binti ya Misri ataibishwa.

Atatiwa mikononi mwa watu wa kaskazini.’^b

25 “Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: ‘Sasa ninamkazia fikira Amoni^c kutoka No,*^d Farao, Misri, miungu yake,^e wafalme wake—naam, Farao na wote wanaomtumaini.’^f

26 “Nami nitawatia mikononi mwa wale wanaotaka kuwaua, mikononi mwa Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni^g na watumishi wake. Lakini baadaye watu watakaa ndani yake kama zamani,’ asema Yehova.’^h

46:21 *Au “kuwajibishwa.” **46:22** *Au “wanaokusanya kuni.” **46:25** *Yaani, Thebesi. **46:26** *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

SURA YA 46

a Yer 46:5, 15

b Eze 30:10

c Nah 3:8

d Eze 30:14

e Kut 12:12
Isa 19:1
Yer 43:12, 13

f Yer 17:5
Yer 42:14

g Yer 43:10, 11
Eze 32:11

h Eze 29:13, 14

Safu ya 2

a Isa 41:13
Isa 43:1, 2
Isa 44:2

b Isa 11:11
Yer 50:19
Eze 39:27
Amo 9:14
Sef 3:20

c Yer 23:3, 6
Yer 30:10, 11

d Yer 25:9

e Yer 5:10
Amo 9:8

f Yer 10:24

SURA YA 47

g Yer 25:17, 20
Eze 25:15, 16
Amo 1:6
Sef 2:4
Zek 9:5, 6

27 ‘Lakini wewe, mtumishi wangu Yakobo, usiogope, Usiwe na hofu, Ee Israeli.^a Kwa maana, nitakuokoa kutoka mbali sana

Na uzao wako* kutoka katika nchi walikopeleka utekwani.^b

Yakobo atarudi na kuwa na utulivu bila usu-mbufu,

Bila mtu wa kuwaogopesha.^c

28 Basi usiogope, mtumishi wangu Yakobo,’ asema Yehova, ‘kwa maana niko pamoja nawe.

Nitayaangamiza kabisa mataifa yote ambako nilikutawanya,^d

Lakini wewe sitakuangamiza.^e

Nitakutia nidhamu* kwa kiwango kinachofaa,^f

Lakini sitakuacha kamwe bila kukuadhibu.”

47 Hili ndilo neno la Yehova kwa nabii Yeremia kuwahusu Wafilisti,^g kabla ya Farao kushambulia Gaza.

2 Yehova anasema hivi:

“Tazama! Maji yanakuja kutoka kaskazini.

Yatakuwa mto unaofurika.

Nayo yataifunika nchi na kila kitu kilichomo,

Jiji na wale wanaokaa humo.

Wanaume watalia kwa sauti,

Na kila mtu anayeishi katika nchi ataomboleza.

3 Watakaposikia sauti ya kishindo cha kwato za farasi dume wake,

46:27 *Tnn., “mbegu yako.” **46:28** *Au “Nitakurekebisha.”

Watakaposikia kelele za magari yake ya vita
Na mvumo wa magurudumu yake,
Akina baba hata hawatageuka kuwatazama wana wao,

Kwa maana mikono yao italegea,

- 4 Kwa sababu siku inayokuja itawaangamiza Wafilisti wote;^a

Itawangamiza kabisa kutoka Tiro^b na kutoka Sidoni^c kila msaidizi aliyebaki.

Kwa maana Yehova atawaangamiza Wafilisti, Ambao wamebaki wa kisiwa cha Kaftori.^{*d}

- 5 Upara^{*} utakuja Gaza. Ashkeloni limenyamazishwa.^e

Ewe uliyebaki katika bonde lao tambarare,^f Utaendelea kujikatakata mpaka lini?^f

- 6 Aha! Upanga wa Yehova!^g Utanyamaza mpaka lini? Rudi ndani ya ala yako. Pumzika na unyamaze.

- 7 Upanga unawezaje kukaa kimya

Wakati Yehova ameuamuru?

Ushambulie Ashkeloni na pwani ya bahari,^h Hapo ndipo alipoupa kazi."

48 Kuhusu Moabu,ⁱ Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi:

"Ole wake Nebo,^j kwa maana ameangamizwa!

47:4 *Yaani, Krete. 47:5 *Yaani, watanoya vichwa vyao kwa kuomboleza na kwa aibu. ^fAu "nchi yao tambarare ya chini."

SURA YA 47

a Yer 25:17, 20
Amo 1:8
Sef 2:5

b Eze 26:2
Amo 1:9, 10

c Isa 23:1, 4
Yer 25:17, 22
Yer 27:2, 3
Eze 28:21
Yoe 3:4

d Mwa 10:13, 14
Kum 2:23

e Sef 2:4

f Kum 14:1
Yer 16:6

g Kum 32:41

h Eze 25:16

SURA YA 48

i Mwa 19:36, 37
Isa 15:1

j Hes 32:37, 38

Safu ya 2

a Yos 13:15, 19
Eze 25:9

b Isa 15:2

c Hes 32:37
Isa 16:8

d Isa 15:5
Yer 48:34

e Isa 15:5

f Hes 21:29
1Fa 11:7

Kiriathaimu^a ameabishwa na kutekwa.

Kimbilio salama limeabishwa* na kuvunjwavunjwa.^b

- 2 Hawamsifu tena Moabu.

Kule Heshboni wamepanga njama ya kumwangusha:^c

'Njoooni, tumkomeshe asiwe taifa.'

Wewe pia, ewe Madmeni, unapaswa kukaa kimya,

Kwa maana upanga unaku fuata.

- 3 Kuna sauti ya kilio kutoka Horonaimu,^d

Ya uharibifu na anguko kubwa.

- 4 Moabu amevunjwa.

Watoto wake wanalia kwa sauti.

- 5 Kwenye njia inayopanda kwenda Luhithi wanaendelea kulia huku wakipanda.

Na kwenye njia inayoshuka kutoka Horonaimu wanasikia vilio vya taabu kwa sababu ya msiba.^e

- 6 Kimbieni, okoeni uhai wenu!^{*}

Ni lazima muwe kama mberoshi nyikani.

- 7 Kwa sababu unatumaini kazi zako na hazina zako,

Wewe pia utatekwa.

Na Kemoshi^f atapelekwa uhamishoni,

Pamoja na makuhani wake na wakuu wake.

- 8 Mwangamizaji atakuja katika kila jiji,

48:1 *Au "Kilele salama kimeabishwa."

48:6 *Au "nafsi zenu."

Na hakuna jiji litakaloponyoka.^a

Hakika bonde litaangamia,*

Na nchi tambarare itahari-biwa,[#] kama alivyosema Yehova.

9 Mwekeeni Moabu alama, Kwa maana atakapoanguka na kuwa magofu atakimbia,

Na majiji yake yatakuwa kitu cha kutisha, Bila mkaaji.^b

10 Alaaniwe mtu anayefanya kazi ya Yehova kwa uze-mbe!

Alaaniwe mtu anayeuzuia upanga wake usimwage damu!

11 Wamoabu hawajasumbuliwa tangu ujana wao, Kama divai iliyotulia kwenye machicha.

Hawajamiminwa kutoka katika chombo kimoja kwenda kingine,

Nao hawajawahi kamwe kupelekwa uhamishoni.

Ndiyo sababu ladha yao imebaki vilevile,

Na harufu yao haijabadilika.

12 “Kwa hiyo tazama! siku zinakuja,” asema Yehova, ‘nitakapowatuma watu wawapindue. Watawapindua na kumwaga kabisa kile kilicho ndani ya vyombo vyao, nao wataivunja mitungi yao mikubwa vipandevipande. **13** Na Wamoabu wataona aibu kwa sababu ya Kemoshi, kama watu wa nyumba ya Israeli wali-vyoona aibu kwa sababu

48:8 *Au “nchi tambarare ya chini itaangamia.”[#] Au “uwanda utaharibiwa.”

SURA YA 48

a Eze 25:9

b Ser 2:9

Safu ya 2

a 1Fa 12:28, 29

Ho 10:15

Amo 5:5

b Isa 16:6

c Yer 48:8

d Isa 34:2

e Zb 24:8

f Eze 25:11

g Hes 21:30

Yos 13:15, 17

Isa 15:2

h Yer 48:8

i Hes 32:34

Kum 2:36

j Hes 21:13

Yos 13:8, 9

ya Betheli, iliyokuwa tegemeo lao.^a

14 Mnawezaje kuthubutu kusema: “Sisi ni mashujaa hodari, walio tayari kwa vita”?^b

15 ‘Moabu ameangamizwa, Majiji yake yamevamiwa,^c Na vijana wao walio bora wamechinjwa,^d Asema Mfalme, ambaye jina lake ni Yehova wa majeshi.^e

16 Msiba wa Wamoabu unakuja hivi karibuni, Na anguko lao linakaribia upesi.^f

17 Wote wanaowazunguka watawasikitikia, Wote wanaolijua jina lao. Waambieni hivi: ‘Jinsi fimbo yenye nguvu ilivyovunjwa, fimbo ya urembo!’

18 Shuka chini kutoka kwenye utukufu wako, Nawe uketi katika kiu,^{*} ewe binti unayekaa Diboni,^g

Kwa maana mwangamizaji wa Moabu amekuja kushambulia, Ataziharibu sehemu zako zenye ngome.^h

19 Simama kando ya barabara utazame, wewe mkaaji wa Aroeri.ⁱ

Muulize mwanamume anayekimbia na mwanamke anayeponyoka. ‘Ni nini ambacho kimetokea?’

20 Moabu ameabishwa na kushikwa na hofu. Omboleza na ulie kwa sauti.

Tangazeni kule Arnoni!

48:18 *Au labda, “kwenye ardhi kavu.”

kwamba Moabu amea-ngamizwa.

21 “Hukumu imekuja kwenye nchi tambarare,*^a dhidi ya Holoni, Yahazi,^b na Mefaathi;^c **22** dhidi ya Diboni,^d Nebo,^e na Beth-diblahaimu;^f **23** dhidi ya Kiriathaimu,^g Beth-gamuli, na Beth-meoni;^g **24** dhidi ya Keriothi^h na Bosra; na dhidi ya majiji yote ya nchi ya Moabu, yaliyo mbali na yaliyo karibu.

25 ‘Nguvu za* Moabu zimekatawa;

Na mkono wake umevunjwa,’ asema Yehova.

26 ‘Mlewesheni,ⁱ kwa maana amejikweza dhidi ya Yehova.^j

Moabu anagaaga katika matapishi yake, Naye ni kitu cha kudhihakiwa.

27 Je, kwako Israeli hakuwa kitu cha kudhihakiwa?^k Je, alipatikana kati ya wezi,

Hivi kwamba utikise kichwa chako na kumshutumu?

28 Ondokeni katika majiji, mkae kwenye jabali, ni nyi wakaaji wa Moabu, Na muwe kama njiwa anayejenga kiota kwenye kuta za korongo.”

29 “Tumesikia kuhusu kiburi cha Moabu—ana majivuno sana—

Kuhusu kujisifu kwake, kiburi chake, majivuno yake, na jinsi moyo wake ulivyotutumuka.”^l

30 “‘Ninajua ghadhabu yake,’ asema Yehova,

SURA YA 48

a Sef 2:9

b Hes 21:23
Isa 15:4

c Yos 13:15, 18

d Hes 32:34

e Hes 32:3, 4

f Hes 32:37
Yer 48:1

g Hes 32:37, 38
Yos 13:15, 17
Eze 25:9

h Amo 2:2

i Yer 25:15, 16

j Yer 48:42

k Omb 2:15
Sef 2:8

l Isa 16:6
Isa 25:10, 11
Sef 2:9, 10

Safu ya 2

a 2Fa 3:24, 25
Isa 16:7

b Hes 21:32
Hes 32:34, 35
Yos 21:8, 39

c Hes 32:37, 38
Yos 13:15, 19

d Isa 16:8, 9
Yer 48:8

e Yer 25:10

f Isa 16:10

g Hes 21:25
Yos 13:15, 17

h Hes 32:37
Isa 16:9

i Hes 21:23

j Yer 48:2, 3

k Isa 15:4-6

‘Lakini maneno yake matupu yatakuwa ya bure. Hayatafanya chochote.

31 Ndiyo sababu nitaiombolezea Moabu,

Nitalia kwa sauti kwa ajili ya Moabu yote

Na kuwaombolezea wa-naume wa Kir-heresi.^a

32 Nitakulilia kwa kilio kinachoshinda kilio cha Yazeri,^b

Nitakulilia, ewe mzabibu wa Sibma.^c

Machipukizi yako yanayositawi yamevuka bahari.

Yamefika mpaka baharini, mpaka Yazeri.

Mwangamizaji ameshuka kwenye

Matunda yako ya wakati wa kiangazi na mavuno yako ya zabibu.^d

33 Furaha na shangwe vi-meondolewa katika shamba la matunda

Na katika nchi ya Moabu.^e Nimefanya divai iache kutiririka kutoka kwenye shinikizo la divai.

Hakuna mtu atakayelikanyaga shinikizo la divai kwa vigelegele vya shangwe.

Watapaza sauti lakini si kwa shangwe.”^f

34 “‘Kuna kilio kikubwa kutoka Heshboni^g mpaka Eleale.^h

Wanapaza sauti yao mpaka Yahazi,ⁱ

Kutoka Soari mpaka Horonaimu,^j mpaka Eglath-shelishiya.

Hata maji ya Nimrimu yatabaki ukiwa.^k

48:21 *Au “uwanda.” 48:25 *Tnn., “Pembe ya.”

- 35** Nitamwondoa kabisa katika Moabu,' asema Yehova,
'Mtu anayeleta toleo mahali pa juu
Na mtu anayemtolea dhambi huu wake.
- 36** Ndiyo sababu moyo wangu utaiombolezea* Moabu kama filimbi,^{#a}
Na moyo wangu utawoimbolezea* wanaume wa Kir-heresi kama filimbi.[#]
Kwa kuwa utajiri aliopata utaangamia.
- 37** Kwa maana kila kichwa kina upara,^b
Na ndevu zote zimenyolewa.
Kila mkono umekatwaka-twa,^c
Nao wamevaa nguo za magunia kiunoni!"^d
- 38** "Juu ya paa zote za Moabu
Na katika viwanja vyake vyote vya jiji,
Hakuna kitu kingine ila maombolezo.
Kwa maana nimemvunja Moabu
Kama chombo kilichotupwa,' asema Yehova.
- 39** 'Jinsi alivyo na hofu! Ombolezeni!
Jinsi Moabu alivyougeuza mgongo wake kwa aibu!
Moabu amekuwa kitu cha kudhihakiwa,
Kitu cha kutisha kwa wote wanaomzunguka."
- 40** "Kwa maana Yehova anasema hivi:

48:36 *Au "utakuwa na msukosuko kwa ajili ya." #Yaani, filimbi iliyopigwa wakati wa kuomboleza kwenye mazishi.

SURA YA 48

a Isa 16:11

b Yer 16:6

c Law 19:28

d Mwa 37:34
Isa 15:2, 3

Safu ya 2

a Omb 4:19
Hab 1:8

b Yer 49:22

c Yer 30:11

d Yer 48:29

e Hes 21:26, 28

f Hes 24:17
Amo 2:2g Hes 21:29
1Fa 11:7

h Yer 48:7

"Tazama! Kama tai anayeshuka chini kwa ghafla,^a
Atanyoosha mabawa yake juu ya Moabu.^b

- 41** Miji itatekwa,
Na ngome zake zitachukuliwa.
Siku hiyo moyo wa mashujaa wa Moabu
Utakuwa kama moyo wa mwanamke anayezaa."^g
- 42** "Na Moabu ataangamizwa asiwe taifa,^c
Kwa maana amejikweza dhidi ya Yehova.^d
- 43** Hofu na shimo na mtego viko mbele yako,
Ewe mkaaji wa Moabu,' asema Yehova.
- 44** 'Yeyote anayekimbia hofu ataanguka shimoni,
Na yeyote anayetoka shimoni atanaswa na mtego.'
'Kwa maana nitawaletea watu wa Moabu mwaka wao wa adhabu,' asema Yehova.
- 45** 'Katika kivuli cha Heshboni, wale wanaokimbia wanasimama wakiwa wameishiwa na nguvu.
Kwa maana moto utatoka Heshboni
Na mwali wa moto utatoka katikati ya Sihoni.^e
Utateketeza kabisa paji la uso wa Moabu
Na fuvu la wana wa ghasia.'^f
- 46** 'Ole wako, ewe Moabu! Watu wa Kemoshi^g wameangamia.
Kwa maana wana wako wamechukuliwa mateka,
Na mabinti zako wamepelekwa uhamishoni.^h

47 Lakini siku za mwisho nitawakusanya watu wa Moabu waliotekwa,' asema Yehova.

'Hukumu ya Moabu imefikia hapa.'^a

49 Kuhusu Waamoni,^b Yehova anasema hivi:

"Je, Israeli hana wana:

Je, hana mrithi?

Kwa nini Malkamu^c amemiliki Gadi?^d

Na kwa nini watu wake wanaishi katika majiji ya Israeli?"

2 "'Kwa hiyo tazameni! siku zinakuja,' asema Yehova,

'Nitakapofanya king'ora cha vita kisikike* dhidi ya jiji la Raba^e la Waamoni.^f

Atakuwa kilima chenye ukiwa,

Na miji yake itawashwa moto.'

'Na Israeli atawamiliki wale walioichukua nchi yake,'^g asema Yehova.

3 'Omboleza, ewe Heshboni, kwa maana Ai ameharibiwa!

Lieni kwa sauti, enyi miji ya Raba.

Vaeni nguu za magunia.

Ombolezeni na mzunguke-zunguke kati ya mazizi ya mawe,*

Kwa maana Malkamu atapelekwa uhamishoni, Pamoja na makuhani wake na wakuu wake.^h

4 Kwa nini unajigamba kuhusu mabonde,*

SURA YA 48

a Eze 25:11

SURA YA 49

b Mwa 19:36, 38
Kum 2:19
2Nya 20:1

c 1Fa 11:5
Sef 1:4, 5

d Amo 1:13

e Kum 3:11
Yos 13:24, 25
Eze 25:5
Amo 1:14

f Eze 21:19, 20

g Isa 14:2
Yer 50:19
Sef 2:9

h Amo 1:13, 15

Safu ya 2

a Mwa 36:10, 11
Eze 25:13
Amo 1:12
Oba 8

b Isa 21:13
Yer 25:17, 23

c Oba 5

Kuhusu eneo lako tambarare linalotiririka, ewe binti usiye mwaminifu, Unayezitumaini hazina zako

Na unayesema: "Ni nani atakayenishambulia?"^a

5 "'Tazama, ninakuletea jambo la kutisha,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi,

'Kutoka kwa wale wote wanaokuzunguka.

Utatawanywa kila upande, Na hakuna atakayewakusanya wale wanaokimbia.'"

6 "'Lakini baadaye nita-wakusanya Waamoni waliotekwa,' asema Yehova."

7 Kuhusu Edomu, Yehova wa majeshi anasema hivi:

"Je, hakuna tena hekima yoyote huko Temani?^a

Je, ushauri mzuri umetoweka kwa wale walio na uelewaji?

Je, hekima yao imeoza?

8 Kimbieni, geukeni!

Nendeni mkakae katika sehemu za chini zenye kina, enyi wakaaji wa Dedani!^b

Kwa maana nitamletea Esau msiba

Wakati wangu wa kumkazia fikira utakapofika.

9 Ikiwa wavunaji wa zabibu wangekuvamia,

Je, hawangeacha zabibu chache za kuokotwa?

Kama wezi wangekuja usiku,

Wangesababisha uharibifu kadiri wapendavyo.^c

49:2 *Au labda, "kelele za vita zisikike."

49:3 *Au "mazizi ya kondoo." 49:4

*Au "maeneo tambarare ya chini."

10 Lakini nitamvua Esau awe uchi.

Nitafichua maficho yake,
Ili asiweze kujificha.

Watoto wake na ndugu
zake na majirani zake
wataangamizwa,^a

Naye hatakuwepo tena.^b

11 Waache mayatima wako,
Nami nitawahifadhi hai,
Na wajane wako watanitu-
maini.”

12 Kwa maana Yehova ana-
sema hivi: “Tazama! Ikiwa
wale ambao hawajahukumiwa
kunywa kikombe lazima waki-
nywe, je, wewe utaachwa ka-
bisa bila kuadhibiwa? Huta-
achwa bila kuadhibiwa, kwa
maana lazima ukinywe.”^c

13 “Kwa maana nimeapa
kwa nafsi yangu mwenyewe,”
asema Yehova, “kwamba Bos-
ra litakuwa kitu cha kutisha,^d
shutuma, uharibifu, na laana;
na majiji yake yote yatakuwa
magofu ya kudumu.”^e

14 Nimesikia habari kutoka
kwa Yehova,
Mjumbe ametumwa kati ya
mataifa aseme hivi:
“Jikusanyeni pamoja na
mumshambulie;
Jitayarisheni ili kupiga-
na.”^f

15 “Kwa maana tazama! Ni-
mekufanya uwe mdogo
sana kati ya mataifa,
Umedharauliwa kati ya
wanadamu.”^g

16 Mtetemeko uliosababisha
umekudanganya,
Kimbelebele cha moyo
wako,
Ewe unayekaa katika ma-
pango ya jabali,
Unayekaa kwenye kilima
kirefu zaidi.

SURA YA 49

a Oba 6, 9

b Mal 1:3, 4

c Yer 25:27, 28
Omb 4:21
Oba 16

d Isa 34:6
Isa 63:1
Yer 49:22
Amo 1:12

e Oba 18
Mal 1:3

f Oba 1

g Oba 2-4

Safu ya 2

a Yer 49:13

b Mwa 19:24, 25

c Isa 34:6, 10

d Yer 4:7

e Zb 76:7
Yer 50:44-46
Nah 1:6

f Oba 9

g Mal 1:4

h 1Fa 9:26

i Yer 4:13

Ingawa unajenga kiota
chako juu kama tai,
Nitakushusha chini kutoka
huko,” asema Yehova.

17 “Na lazima Edomu awe
kitu cha kutisha.”^a Kila mtu
anayepita kando yake atataza-
ma kwa hofu na kupiga
mluzi kwa sababu ya mapigo
yake yote. **18** Kama Sodoma
na Gomora na miji jirani ili-
vyoangamizwa,”^b Yehova ana-
sema, “hakuna mtu atakaye-
kaa huko, na hakuna mtu ata-
kayeishi huko.”^c

19 “Tazameni! Kama simba
anayetoka kwenye vichaka^d
vikubwa kando ya Yorda-
ni, mtu fulani atayashambu-
lia malisho yaliyo salama, la-
kini kwa muda mfupi nita-
mfanya Edomu akimbie kuto-
ka nchini. Nami nitaweka juu
ya nchi hiyo yule aliyechagu-
liwa. Kwa maana ni nani aliye
kama mimi, na ni nani ataka-
yenipinga? Ni mchungaji gani
anayeweza kusimama mbele
zangu?”^e **20** Kwa hiyo sikieni,
enyi watu, uamuzi ambao* Ye-
hova amefanya dhidi ya Edo-
mu na mawazo yake dhidi ya
wakaaji wa Temani:^f

Hakika walio wadogo kati-
ka kundi watakokotwa.

Atayafanya makao yao
yawe ukiwa kwa sababu
yao.^g

21 Dunia imetetemeka kwa
sauti ya kuanguka kwao.
Kuna kilio kikubwa!
Sauti imesikika mpaka
kwenye Bahari
Nyekundu.^h

22 Tazameni! Atateremka na
kushuka kwa ghafla
kama tai,ⁱ

49:20 *Au “shauri ambalo.”

Naye atanyoosha mabawa yake juu ya Bosra.^a

Siku hiyo moyo wa mashujaa wa Edomu

Utakuwa kama moyo wa mwanamke anayezaa.”

23 Kuhusu Damasko:^b

“Hamathi^c na Arpadi wameaibishwa,

Kwa maana wamesikia habari mbaya.

Wanayeyuka kwa woga.

Kuna msukosuko baharini ambao hauwezi kutuli zwa.

24 Damasko amekufa moyo.

Amegeuka ili kukimbia, lakini ameshikwa na hofu.

Ampatwa na taabu na uchungu,

Kama mwanamke anayezaa.

25 Kwa nini jiji lenye sifa halijaachwa,

Mji wa furaha?

26 Kwa maana vijana wake wataanguka katika viwanja vyake vya jiji,

Na wanajeshi wote wataangamia siku hiyo,” asema Yehova wa majeshi.

27 “Nitauwasha moto ukuta wa Damasko,

Nao utaiteketeza kabisa minara yenye ngome ya Ben-hadadi.”^d

28 Kuhusu Kedari^e na falme za Hasori, ambazo Mfalme Nebukadnezah* wa Babiloni alizishambulia na kuzishinda, Yehova anasema hivi:

“Inukeni, pandeni mwende Kedari,

49:28, 30 *Tnn., “Nebukadrezah,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

SURA YA 49

a Yer 48:40
Yer 49:13

b Isa 17:1
Amo 1:3

c Hes 13:21
2Fa 17:24
Zek 9:1, 2

d Amo 1:4

e Mwa 25:13
Isa 42:11
Isa 60:7
Eze 27:21

Safu ya 2

a Yer 9:25, 26
Yer 25:17, 23

Na muwaangamize wana wa Mashariki.

29 Mahema yao na mifugo yao itachukuliwa, Vitambaa vyao vya mahema na mali zao zote.

Ngamia wao watachukuliwa,

Nao watawalilia, ‘Kuna hofu kila mahali!’”

30 “Kimbieni, nendeni mbali sana!

Nendeni mkae katika sehemu za chini zenye kina, enyi wakaaji wa Hasori,” asema Yehova.

“Kwa maana Mfalme Nebukadnezah* wa Babiloni ametunga mbinu dhidi yenu,

Naye amefanya mpango wa kuwashambulia.”

31 “Inukeni, shambulieni taifa lililo na amani,

Linalokaa kwa usalama!” asema Yehova.

“Halina milango wala makomeo; wanaishi peke yao.

32 Ngamia wao wataporwa, Na mifugo yao mingi itakuwa nyara.

Nitawatawanya kwa kila upepo,*

Wale ambao wananyoa nywele pembeni mwa vichwa vyao,^a

Nami nitaleta msiba wao kutoka kila upande,” asema Yehova.

33 “Na Hasori atakuwa pango la mbwa mwitu, Ukiwa wa kudumu.

Hakuna mtu atakayekaa huko,

49:32 *Au “kila upande.”

Na hakuna mtu atakayei-shi ndani yake.”

34 Hili ndilo neno la Yehova lililomjia nabii Yeremia kuhusu Elamu^a mwanzoni mwa utawala wa Mfalme Sedekia^b wa Yuda: **35** “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Ninauvunjia upinde wa Elamu,^c chanzo cha* nguvu zao. **36** Nitaleta juu ya Elamu zile pepo nne kutoka kwenye miisho minne ya mbingu, nami nitawatawanya kwenye pepo hizi zote. Hakuna taifa ambako watu wa Elamu waliotawanywa hawataenda.”

37 “Nitawavunjavunja Waelamu mbele ya maadui wao na mbele ya wale wanaotaka kuwaua; nami nitawaletsa msiba, hasira yangu inayowaka,” asema Yehova. “Nami nitautuma upanga uwafuate mpaka nitakapowaangamiza kabisa.”

38 “Nami nitaweka kiti changu cha ufalme huko Elamu,^d na huko nitamwangamiza mfalme na wakuu,” asema Yehova.

39 “Lakini siku za mwisho, nitawakusanya watu wa Elamu waliotekwa,” asema Yehova.

50 Neno ambalo Yehova alisema kuhusu Babiloni,^e kuhusu nchi ya Wakaldayo, kupitia nabii Yeremia:

2 “Semeni jambo hili kati ya mataifa na mlitangaze. Inueni ishara* na mlitangaze. Msifiche jambo lolote! Semeni, ‘Babiloni ametekwa.’^f Beli ameabishwa.^g

49:35 *Tnn., “mwanzo wa.” 50:2 *Au “nguzo ya ishara.”

SURA YA 49

a Mwa 10:22
Isa 21:2
Yer 25:17, 25
Eze 32:24
Da 8:2
Mdo 2:8, 9

b 2Fa 24:18

c Isa 22:6

d Yer 25:17, 25

SURA YA 50

e Isa 13:1

f Yer 51:8
Ufu 14:8

g Isa 46:1
Yer 51:44

Safu ya 2

a Isa 13:17
Yer 51:11, 48

b Isa 11:12
Yer 3:18
Ho 1:11

c Yer 31:8, 9

d Ho 3:5

e Isa 35:10

f Yer 31:31

g Isa 53:6

h Yer 10:21
Yer 23:2
Eze 34:2, 6

i Zb 79:6, 7

Merodaki ameshikwa na hofu.

Sanamu zake zimeabi-shwa.

Sanamu zake zinazochukiza* zimeshikwa na hofu.”

3 Kwa maana taifa lime-mshambulia kutoka kaskazini.^a

Linaifanya nchi yake kuwa kitu cha kutisha;

Hakuna mtu anayekaa ndani yake.

Mwanadamu na pia mnyama wamekimbia;

Wameenda zao.”

4 “Siku hizo na wakati huo,” asema Yehova, “watu wa Israeli na watu wa Yuda watakuja pamoja.^b Watatembea wakilia,^c na pamoja watamtafuta Yehova Mungu wao.^d

5 Watauliza njia ya kwenda Sayuni, nyuso zao zikiwa zimeelekezwa upande huo,^e wakisema, ‘Njooi, tujiunge na Yehova katika agano la milele ambalo halitasahauliwa.’^f

6 Watu wangu wamekuwa kundi la kondoo walipotee.^g Wachungaji wao wenyewe waliwafanya wapotee.^h

Waliwapeleka kwenye milima, wakitangatanga kutoka mlima mpaka kilima. Wamepasahau mahali pao pa kupumzika. **7** Wale wote wanaowapata wamewanyafua,ⁱ na maadui wao wamesema, ‘Hatuna hatia, kwa sababu walimtendea dhambi Yehova, walimtendea dhambi Yehova ambaye ni makao ya uadilifu na tumaini la mababu zao.’”

50:2 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

- 8** “Kimbieni kutoka Babiloni,
Tokeni katika nchi ya Wakkaldayo,^a
Na muwe kama wanyama
wanaolitangulia kundi.
- 9** Kwa maana sasa ninamsha na kuleta dhidi ya Babiloni
Kusanyiko la mataifa makubwa kutoka katika nchi ya kaskazini.^b
Watamshambulia wakiwa wamejipanga kivita;
Kutoka hapo atatekwa.
Mishale yao ni kama ya shujaa
Inayosababisha wazazi wafiwe na watoto;^c
Hairudi bila matokeo.
- 10** Ukaldayo itakuwa nyara.^d
Wale wote wanaochukua nyara kutoka kwake watahuba kabisa,^e asema Yehova.
- 11** “Kwa maana mliendelea kushangilia,^f mliendelea kufurahi
Mlipokuwa mkiupora urithi wangu mwenyewe.^g
Kwa maana mliendelea kukanyagakanyaga kama ndama jike kwenye nyasi,
Nanyi mkaendelea kulia kama farasi dume.
- 12** Mama yenu ameabishwa.^h
Yule aliyewazaa amekata tamaa.
Tazameni! Yeye ndiye mdogo zaidi kati ya mataifa,
Nyika isiyo na maji na ambayo ni jangwa.ⁱ
- 13** Kwa sababu ya ghadhabu ya Yehova hatakaliwa;^j
Atakuwa ukiwa kabisa.^k
Yeyote anayepita kando ya

SURA YA 50

a Isa 48:20
Yer 51:6, 45
Zek 2:7
2Ko 6:17
Ufu 18:2, 4

b Isa 21:2
Yer 51:11, 27,
28, 48
Da 5:28, 30

c Isa 13:17, 18

d Yer 25:12
Yer 27:6, 7

e Ufu 17:16

f Omb 1:21

g Isa 14:4-6
Isa 47:6
Yer 30:16

h Isa 47:8

i Isa 13:20, 21

j Zek 1:15

k Yer 25:12

Safu ya 2

a Yer 51:37

b Isa 13:18
Yer 51:11

c Yer 51:35, 36

d Yer 51:58

e Yer 51:6, 11

f Zb 137:8
Ufu 18:6

g Yer 51:23

h Isa 13:14
Yer 51:9

i Yer 23:1
Yer 50:6
Eze 34:5

j Yer 2:15

k 2Fa 17:6
Isa 8:7

l 2Fa 25:1
2Nya 36:17
Yer 4:7

Babiloni atatazama kwa hofu

Na kupiga mluzi kwa sababu ya mapigo yake yote.^a

- 14** Mshambulieni Babiloni mkiwa mmejipanga kivita kila upande,
Ninyi nyote mnaoupinda* upinde.

Mpigieni mishale, msiuache mishale wowote,^b

Kwa maana amemtendea dhambi Yehova.^c

- 15** Mpigieni kelele za vita kila upande.

Amejisalimisha.*

Nguzo zake zimeanguka, kuta zake zimebomolewa,^d

Kwa maana ni kisasi cha Yehova.^e

Jilipizieni kisasi dhidi yake.

Mtendeeni kama alivyotenda.^f

- 16** Mkatilieni mbali mpandaji wa mbegu kutoka Babiloni

Na yule anayebeba mundu wakati wa mavuno.^g

Kwa sababu ya upanga ulio katili, kila mtu atarudi kwa watu wake mwenyewe,

Kila mtu atakimbilia nchi yake mwenyewe.^h

- 17** “Watu wa Israeli ni kondooⁱ waliotawanyika. Simba wamewatawanya.^j Kwanza mfalme wa Ashuru aliwanya-fua;^k kisha Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni akaguguna mifupa yao.^l **18** Kwa hiyo Yehova wa majeshi, Mungu wa

50:14 *Tnn., “mnaoukanyaga.” **50:15** *Tnn., “Amempa mkono wake.” **50:17** *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

Israeli, anasema hivi: 'Nita-
mtendea mfalme wa Babilo-
ni na nchi yake kama nilivyo-
mtendea mfalme wa Ashuru.^a

19 Nami nitamrudisha Israe-
li kwenye malisho yake,^b naye
atalisha juu ya Karmeli na juu
ya Bashani,^c naye atashiba
kwenye milima ya Efraimu^d na
ya Gileadi."^e

20 "Siku hizo na wakati huo,"
asema Yehova,
"Hatia ya Israeli itatafu-
twa,
Lakini hakutakuwa na ha-
tia yoyote,
Na dhambi za Yuda hazita-
patikana,
Kwa maana nitawasamehe
wale nitakaowaacha wa-
baki."^f

21 "Panda ukashambulie
nchi ya Merathaimu na
wakaaji wa Pekodi.^g
Acha wauawe na kuanga-
mizwa* kabisa," asema
Yehova.
"Fanya yote niliyokua-
muru.

22 Kuna sauti ya vita nchini,
Msiba mkubwa.

23 Jinsi nyundo ya chuma ya
dunia yote ilivyokatwa
na kuvunjwa!^h
Jinsi ambavyo Babiloni
amekuwa kitu cha kuti-
sha kati ya mataifa!ⁱ

24 Nimekutegea mtego, nawe
umenaswa, Ee Babiloni,
Nawe hukujua.
Ulipatikana na kukama-
twa,^j
Kwa maana ulimpinga Ye-
hova.

25 Yehova amefungua ghala
lake,

SURA YA 50

a 2Fa 19:35
Isa 14:25
Sef 2:13

b Isa 11:16
Isa 65:10
Yer 23:3
Yer 33:7
Eze 34:14
Mik 2:12

c Mik 7:14

d Yer 31:6

e Oba 19

f Isa 44:22
Yer 31:34
Mik 7:19

g Eze 23:22, 23

h Isa 14:5, 6
Yer 51:20

i Yer 51:41
Ufu 18:15, 16

j Yer 51:31
Da 5:30
Ufu 18:8

Safu ya 2

a Isa 13:5
Yer 51:11

b Yer 51:27

c Yer 50:10

d Isa 14:22, 23

e Isa 34:6, 7
Eze 39:18

f Zb 94:1
Yer 51:11

g Yer 50:14

h Zb 137:8
Yer 51:56

i Omb 3:64
Ufu 18:6

j Isa 14:13

Naye anatoa silaha za gha-
dhabu yake.^a

Kwa maana Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu, Yehova wa
majeshi, ana kazi
Katika nchi ya Wakaldayo.

26 Mshambulieni kutoka se-
hemu za mbali.^b

Fungueni maghala yake.^c
Mrundikeni kama maru-
ndo ya nafaka.

Mwangamizeni kabisa.^d

Naye asiwe na mtu yeyote
anayebaki.

27 Waueni ng'ombe dume
wake wote wachanga;^e
Na washuke kwenda ma-
chinjioni.

Ole wao, kwa maana siku
yao imefika,
Wakati wao wa kuadhibi-
wa!^f

28 Kuna sauti ya wale wanao-
kimbia,
Wale wanaoponyoka kuto-
ka nchi ya Babiloni,
Ili kutangaza katika Sa-
yuni kisasi cha Yehova
Mungu wetu,
Kisasi kwa ajili ya hekalu
lake.^g

29 Waiteni wapiga-mishale
dhidi ya Babiloni,
Wote wanaoupinda* upi-
nde.^h

Pigeni kambi kumzungu-
ka; msiache yeyote
aponyoke.

Mlipeni kulingana na ma-
tendo yake.ⁱ

Mtendeeni kama alivyote-
nda,^j

Kwa maana ametenda kwa
kiburi dhidi ya Yehova,
Dhidi ya Mtakatifu wa
Israeli.^k

50:27 *Au "kuwajibishwa." 50:29
*Tnn., "wanaoukanyaga."

50:21 *Au "uwaangamize."

30 Basi vijana wake wataanguka katika viwanja vyake vya jiji,^a

Na wanajeshi wake wote wataangamia* siku hiyo,” asema Yehova.

31 “Tazama! Niko dhidi yako,^b ewe mkaidi,”^c asema Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, “Kwa maana lazima siku yako itakuja, wakati ambapo nitakufanya uwajibike.*

32 Wewe, ewe mkaidi, utajikwa na kuanguka, Hakutakuwa na mtu wa kukuinua.^d Nami nitayawasha moto majiji yako, Nao utateketeza kabisa kila kitu kinachokuzunguka.”

33 Yehova wa majeshi anasema hivi:

“Watu wa Israeli na Yuda wamekandamizwa, Na wale wote wanaowachukua mateka wamewazuilia.^e Wamekataa kuwaachilia waende.^f

34 Lakini Mkombozi wao ananguvu.^g

Yehova wa majeshi ndilo jina lake.^h

Bila shaka atatetea kesi yao,ⁱ

Ili kuipumzisha nchi^j Na kuwafadhaisha wakaaji wa Babiloni.”^k

35 “Kuna upanga dhidi ya Wakaldayo,” asema Yehova,

50:30 *Tnn., “watanyamazishwa.”

50:31 *Au “wakati ambao nitakua-dhibu.”

SURA YA 50

a Isa 13:17, 18

b Yer 51:25

c Isa 14:13
Da 4:30

d Yer 51:26

e Isa 47:6

f Isa 14:17

g Isa 41:14
Ufu 18:8

h Isa 47:4

i Omb 3:59

j Isa 14:3, 4

k Yer 51:24

Safu ya 2

a Isa 47:13
Yer 51:57
Da 5:7

b Yer 51:30

c Isa 13:8

d Isa 45:3

e Isa 44:27
Yer 51:36, 37
Ufu 16:12

f Isa 46:1
Yer 51:44, 52
Da 5:1, 4

g Isa 13:20, 21
Yer 51:37
Ufu 18:2

h Yer 25:12
Yer 51:43, 64

i Isa 13:19

j Mwa 19:24, 25
Yud 7

k Yer 51:26

“Dhidi ya wakaaji wa Babiloni na dhidi ya wakuu wake na dhidi ya watu wake wenye hekima.^a

36 Kuna upanga dhidi ya wale wanaoongea maneno matupu,* nao watatenda kipumbavu.

Kuna upanga dhidi ya mashujaa wake, nao watashikwa na hofu.^b

37 Kuna upanga dhidi ya farasi wao na magari yao ya vita,

Na dhidi ya watu wa mataifa mbalimbali waliochangamana nao, Nao watakuwa kama wana-wake.^c

Kuna upanga dhidi ya hazina zake, nazo zita-porwa.^d

38 Kuna uharibifu dhidi ya maji yake, nayo yatakau-shwa.^e

Kwa maana ni nchi ya sanamu za kuchongwa,^f

Na kwa sababu ya maono yao yanayotisha wana-endelea kutenda kiwazimu.

39 Kwa hiyo, viumbe wa janguwani watakaa pamoja na wanyama wanaopiga mayowe,

Na mbuni watakaa ndani yake.^g

Hakutakuwa na wakaaji tena ndani yake,

Wala watu hawataishi humo kwa vizazi vyote.”^h

40 “Kama Mungu alivyoa-ngamiza Sodoma na Gomoraⁱ na miji jirani,”^j asema Yehova, “hakuna mtu atakayekaa huko, na hakuna mtu atakayeishi huko.^k

50:36 *Au “manabii wa uwongo.”

- 41** Tazama! Watu wanakuja kutoka kaskazini; Taifa kubwa na wafalme wakuu^a watainuliwa Kutoka sehemu za mbali zaidi za dunia.^b
- 42** Wanatumia upinde na mkuki.^c Ni wakatili na hawataonyesha rehema.^d Sauti yao ni kama bahari inayovuma,^e Wakiwa wamepanda farasi wao. Wamejipanga kivita kama mtu mmoja dhidi yako, ewe binti ya Babiloni.^f
- 43** Mfalme wa Babiloni amesikia habari kuwahusu,^g Na mikono yake imelegea.^h Amapata maumivu, Uchungu kama wa mwana-mke anayezaa.
- 44** "Tazama! Kama simba anayetoka kwenye vichaka vikubwa kando ya Yordani, mtu fulani atayashambulia malisho yaliyo salama, lakini kwa muda mfupi nitawafanya Waedomu wakimbie kutoka nchini. Nami nitaweka juu ya nchi hiyo yule aliyechaguliwa.ⁱ Kwa maana ni nani aliyekama mimi, na ni nani atakayenipinga? Ni mchungaji gani anayeweza kusimama mbele zangu?^j **45** Kwa hiyo sikieni, enyi watu, uamuzi ambao* Yehova amefanya dhidi ya Babiloni^k na mawazo yake dhidi ya nchi ya Wakaldayo. Hakika walio wadogo katika kundi watakokotwa. Atayafanya makao yao yabaki ukiwa kwa sababu yao.^l

50:45 *Au "shauri ambalo."

SURA YA 50

a Isa 45:1
Yer 51:11
Yer 51:27, 28

b Isa 13:5, 17

c Yer 50:9

d Zb 137:8
Isa 13:17, 18

e Yer 51:42

f Yer 51:27

g Yer 51:31

h Da 5:6

i Isa 41:25

j Yer 49:19-21

k Yer 51:11

l Isa 13:1, 20
Yer 51:43

Safu ya 2

a Ufu 18:9

SURA YA 51

b Yer 50:9

c Yer 50:14, 29

d Isa 13:17, 18
Yer 50:30

e Isa 13:15

f Zb 94:14
Isa 44:21
Yer 46:28
Zek 2:12

g Yer 50:8
Zek 2:7
Ufu 18:4

- 46** Sauti ya kutekwa kwa Babiloni itafanya dunia itetememe, Na kilio kitasikika kati ya mataifa."^a

51 Yehova anasema hivi: "Tazameni, ninaleta upepo unaoharibu

Dhidi ya Babiloni^b na dhidi ya wakaaji wa Leb-kamai.*

2 Nitawatuma wapepetaji Babiloni,

Nao watampepeta na kufanya nchi yake kuwa tupu;

Watamshambulia kutoka pande zote siku ya msiba.^c

3 Anayepiga mishale asiupinde* upinde wake.

Na yeyote asisimame akiwa amevaa koti lake la vita.

Msiwahurumie vijana wake.^d

Angamizeni jeshi lake lote.

4 Nao watauawa katika nchi ya Wakaldayo,

Wakiwa wamechomwa kwa silaha katika barabara zake.^e

5 Kwa maana Mungu wa Israeli na Yuda, Yehova wa majeshi, hajawaacha wakiwa wajane.^f

Lakini nchi yao* imejaa hatia machoni pa Mtakatifu wa Israeli.

6 Kimbieni kutoka Babiloni, Kimbieni ili mwokoe uhai wenu.*^g

Msiangamie kwa sababu ya kosa lake.

51:1 *Inaonekana hili ni jina la siri la Ukaldayo. 51:3 *Tnn., "asiukanyage." 51:5 *Yaani, nchi ya Wakaldayo. 51:6 *Au "nafsi yenu."

Kwa maana ni wakati wa kisasi cha Yehova.

Anamlipa kulingana na matendo yake.^a

- 7** Babiloni amekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa Yehova; Aliileweshwa dunia yote. Mataifa yamekunywa divai yake;^b

Ndiyo sababu mataifa yamehikwa na wazimu.^c

- 8** Babiloni ameinguka ghafla, naye amevunjika.^d Mwombolezeeni!^e Leteni zeri kwa ajili ya maumivu yake; labda atapona.”

- 9** “Tulijaribu kumponya Babiloni, lakini hakupona. Mwacheni, twendeni kila mmoja kwenye nchi yake.^f

Kwa maana hukumu yake imefika mbinguni;

Iko juu kama mawingu.^g

- 10** Yehova ametutendea haki.^h

Njooni, tusimulie katika Sayuni kazi ya Yehova Mungu wetu.”ⁱ

- 11** “Isugueni mishale;^j chukueni ngao za mviringo.* Yehova ameichochea roho ya wafalme wa Wamedi,^k Kwa sababu anakusudia kuiangamiza Babiloni. Kwa maana hiki ndicho kisasi cha Yehova, kisasi kwa ajili ya hekalu lake.

- 12** Inueni ishara*^l dhidi ya kuta za Babiloni. Imarisheni ulinzi, wekeni walinzi. Watayarisheni wale wa-naovizia.

51:11 *Au labda, “jazeni podo.” 51:12 *Au “nguzo ya ishara.”

SURA YA 51

a Yer 25:12, 14
Yer 50:15

b Ufu 17:1, 2
Ufu 18:3

c Yer 25:15, 16

d Isa 21:9
Isa 47:9
Ufu 14:8

e Ufu 18:2, 9

f Isa 13:14

g Ufu 18:4, 5

h Mik 7:9

i Yer 50:28

j Yer 50:14

k Isa 13:17
Isa 45:1

l Isa 13:2

Safu ya 2

a Ufu 17:17

b Ufu 17:1, 15

c Isa 45:3
Yer 50:37

d Hab 2:9
Ufu 18:11, 12
Ufu 18:19

e Yer 50:15

f Zb 93:1
Zb 104:24

g Zb 136:5
Met 3:19
Isa 40:22
Yer 10:12-16

h Zb 135:7

i Isa 44:11

j Hab 2:19

Kwa maana Yehova ametunga mbinu, Naye atatekeleza alichohidi dhidi ya wakaaji wa Babiloni.”^a

- 13** “Ewe mwanamke unaye-kaa juu ya maji mengi,^b Mwenye hazina nyingi,^c Mwisho wako umefika, kikomo* chako cha kupata faida.^d

- 14** Yehova wa majeshi amepa kwa nafsi yake, ‘Nitakujaza wanaume wengi kama nzige, Nao watapiga kelele za ushindi juu yako.’^e

- 15** Yeye ndiye Muumba wa dunia kwa nguvu zake, Yule aliyeiimarisha ardhi inayozaa kwa hekima yake^f

Na aliyezitandaza mbingu kwa uelewaji wake.^g

- 16** Anapofanya sauti yake isikike, Maji yaliyo mbinguni huwa na msukosuko, Naye huyafanya mawingu yapande* kutoka kwenye miisho ya dunia. Hutengeneza radi^h kwa ajili ya mvua, Naye huutoa upepo katika maghala yake.^h

- 17** Kila mtu anatenda bila kutumia akili na bila ujuzi. Kila fundi wa chuma ataaibishwa kwa sababu ya sanamu ya kuchongwa;ⁱ Kwa maana sanamu yake ya chuma* ni uwongo, Nazo hazina roho* ndani yake.^j

51:13 *Tnn., “kipimo.” 51:16 *Au “hufanya mvuke upande.” ^aAu labda, “malango.” 51:17 *Au “sanamu yake ya kuyeyushwa.” ^aAu “pumzi.”

- 18** Sanamu hizo ni udangan-yifu, *^a kazi ya mzaha. Siku yao ya hukumu itakapofika, zitaangamia.
- 19** Fungu la Yakobo si kama vitu hivyo,
Kwa maana Yeye ndiye aliyeumba kila kitu,
Hata fimbo ya urithi wake.^b
Yehova wa majeshi ndilo jina lake.”^c
- 20** “Wewe ni rungu langu la vita, silaha ya vita,
Kwa maana nitakutumia kuyavunjavunja mataifa. Nitakutumia kuziangamiza falme.
- 21** Nitakutumia kumvunjavunja farasi na mpandaji wake.
Nitakutumia kulivunjavunja gari la vita na mwendeshaji wake.
- 22** Nitakutumia kumvunjavunja mwanamume na mwanamke.
Nitakutumia kumvunjavunja mzee na mvulana.
Nitakutumia kumvunjavunja mwanamume na mwanamke kijana.
- 23** Nitakutumia kumvunjavunja mchungaji na mifugo yake.
Nitakutumia kumvunjavunja mkulima na kundi lake la wanyama.
Nitakutumia kuwavunjavunja magavana na watawala wasaidizi.
- 24** Nami nitamlipa Babiloni na wakaaji wote wa Ukal-dayo
Kwa sababu ya uovu wote ambao wametenda huko

51:18 * Au “ubatili.”

SURA YA 51

a Isa 41:29
Yer 14:22

b Kum 32:9

c Isa 47:4

Safu ya 2

a Zb 137:8

b Yer 50:31

c Yer 25:9

d Yer 50:13, 40
Ufu 18:21

e Isa 13:2
Yer 51:12

f Mwa 8:4

g Mwa 10:2, 3
Yer 50:41

h Isa 13:17
Da 5:30, 31

Sayuni mbele ya macho yenu,”^a asema Yehova.

- 25** “Tazama, niko dhidi yako,^b ewe mlima wa uharibifu,” asema Yehova,
“Wewe unayeiharibu dunia yote.^c
Nitaunyoosha mkono wangu dhidi yako na kukubingirisha kutoka kwenye majabali
Na kukufanya uwe mlima ulioteketezwa kabisa.”
- 26** “Watu hawatachukua kutoka kwako jiwe la pembeni wala jiwe la msingi,
Kwa sababu utabaki ukiwa milele,”^d asema Yehova.
- 27** “Inueni ishara * katika nchi.^e
Pigeni pembe kati ya mataifa.
Wekeni^f mataifa ya kumshambulia.
Iteni dhidi yake falme za Ararati,^f Mini, na Ashkenazi.^g
Wekeni juu yake ofisa mwandikishaji.
Wafanyeni farasi waje kama nzige wenye miiba.
- 28** Wekeni^f mataifa ya kumshambulia,
Wafalme wa Umedi,^h magavana wake na watawala wake wote wasaidizi
Na nchi zote wanazozitawala.
- 29** Nayo dunia itatetemeka na kutikisika,
Kwa maana mawazo ya Yehova dhidi ya Babiloni yatatekelezwa

51:27 * Au “nguzo ya ishara.” 51:27, 28
^f Tnn., “Takaseni.”

- Ili kuifanya nchi ya Babiloni kuwa kitu cha kutisha, bila mkaaji.^a
- 30** Mashujaa wa Babiloni wameacha kupigana. Wanaketiki kwenye ngome zao. Nguvu zao zimekwisha.^b Wamekuwa kama wanawake.^c Nyumba zake zimewashwa moto. Makomeo yake yamevunjwa.^d
- 31** Mleta habari mmoja anakimbia kukutana na mleta habari mwingine, Na mjumbe mmoja kukutana na mjumbe mwingine, Ili kumjulisha mfalme wa Babiloni kwamba jiji lake limetekwa kila upande,^e
- 32** Kwamba vivuko vimetekwa,^f Kwamba mashua za mafunjo zimeteketewa kwa moto, Na kwamba wanajeshi wana hofu.”
- 33** Kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi:
“Binti ya Babiloni ni kama uwanja wa kupuria. Ni wakati wa kumkanyagia chini awe mgumu. Hivi karibuni wakati wake wa mavuno utafika.”
- 34** “Mfalme Nebukadreza* wa Babiloni ameninyafua;^g Amenivuruga. Ameniiweka chini kama chombo kitupu. Amenimeza kama nyoka mkubwa;^h

51:34 * Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili.

SURA YA 51

- a Isa 13:13, 19
Yer 50:13
Yer 50:39, 40
- b Isa 13:7
- c Yer 50:37
- d Zb 107:16
Isa 45:2
- e Isa 47:11
Yer 50:24, 43
- f Isa 44:27
Yer 50:38
Ufu 16:12
- g 2Nya 36:17, 18
Yer 50:17
- h Yer 51:44
- Safu ya 2
- a Zb 137:8
Yer 50:29
- b Yer 50:34
- c Kum 32:35
- d Isa 44:27
Yer 50:38
- e Yer 25:12
Yer 50:15
- f Isa 13:19, 22
- g Yer 50:13, 39
- h Da 5:1, 4
- i Yer 25:17, 27
Yer 51:57

j Yer 25:17, 26

- Amelijaza tumbo lake kwa vitu vyangu vizuri. Amenioshea mbali.
- 35** ‘Babiloni na alipizwe kwa sababu ya ukatili niliotendewa mimi na mwili wangu!’ asema mkaaji wa Sayuni.^a
‘Na wakaaji wa Ukaldayo na walipizwe kwa sababu ya damu yangu!’ asema Yerusalemu.”
- 36** Kwa hiyo Yehova anasema hivi:
“Ninaitetea kesi yako,^b Nami nitakulipizia kisasi.^c Nitaikausha bahari yake na kuvikausha visima vyake.^d
- 37** Na Babiloni atakuwa marundo ya mawe,^e Pango la mbwa mwitu,^f Kitu cha kutisha na kitu cha kupigiwa mluzi, Bila mkaaji.^g
- 38** Wote pamoja watanguruma kama wanasimba.* Watanguruma kama watooto wa simba.”
- 39** “Watakapokuwa wamesisimka, nitaandaa karamu yao na kuwaleweshwa, Ili wafurahi;^h Kisha watalala usingizi wa kudumu, Nao hawataamka kutoka katika usingizi huo,ⁱ asema Yehova.
- 40** “Nitawashusha chini kama wanakondoo kwenda machinjioni, Kama kondoo dume pamoja na mbuzi.”
- 41** “Jinsi Sheshaki* alivyotekwa,^j

51:38 *Au “wanasimba wenye manyoya marefu shingoni.” 51:41 *Inaonekana hili ni jina la siri la Babeli (Babiloni).

Jinsi Sifa ya dunia yote ilivyokamatwa!^a

Jinsi ambavyo Babiloni amekuwa kitu cha kutisha kati ya mataifa!

42 Bahari imekuja juu ya Babiloni.

Mawimbi yake mengi yamemfunika.

43 Majiji yake yamekuwa kitu cha kutisha, nchi isiyo na maji na jangwa.

Nchi ambayo hakuna mtu atakayeishi wala kupitia humo.^b

44 Nitamkazia fikira Beli^c huko Babiloni, Nami nitatoa kinywani mwake kile alichomeza.^d Mataifa hayatamiminika kwake tena.

Na ukuta wa Babiloni utainguka.^e

45 Tokeni kati yake, watu wangu!^f

Kimbieni ili mwokoe uhai wenu^{*g} kutoka kwa hasira ya Yehova inayowaka!^h

46 Msife moyo wala msiohope kwa sababu ya habari itakayosikiwa nchini.

Katika mwaka mmoja habari itakuja,

Na mwaka unaofuata habari nyingine,

Kuhusu ukatili nchini na kuhusu mtawala aki-mshambulia mtawala mwingine.

47 Kwa hiyo tazama! siku zinakuja

Nitakapozikazia fikira sanamu za kuchongwa za Babiloni.

Nchi yake yote itaabiishwa,

SURA YA 51

a Isa 13:19
Yer 49:25
Da 4:30

b Isa 13:1, 20
Yer 50:39

c Isa 46:1
Yer 50:2

d 2Nya 36:7
Ezr 1:7
Yer 51:34
Da 1:1, 2

e Yer 51:58

f Isa 48:20
Ufu 18:4

g Yer 51:6
Zek 2:7

h Isa 13:13

Safu ya 2

a Isa 13:15
Da 5:30

b Isa 44:23
Isa 48:20
Isa 49:13
Ufu 18:20

c Yer 50:3
Yer 50:41

d Yer 50:17
Yer 51:24

e Yer 50:8
Ufu 18:4

f Ezr 1:3
Zb 137:5

g Zb 79:1
Omb 1:10

h Isa 13:15

i Isa 14:13
Da 4:30

Na watu wake wote waliouawa wataanguka ndani yake.^a

48 Mbingu na dunia na vyote vilivyomo

Vitapiga vigelegele vya shangwe kwa sababu ya Babiloni,^b

Kwa maana waangamizaji watamvamia kutoka kaskazini,^{*c} asema Yehova.

49 "Babiloni hokusababisha tu kuuawa kwa Waisraeli walioanguka^d

Bali pia huko Babiloni watu waliouawa wa dunia yote wameanguka.

50 Ninyi mnaoponyoka upanga, endeleeni kupiga mwendo, msisimame tuli!^e

Mkumbukeni Yehova kutoka mbali,

Yerusalem na aingie moyoni mwenu."^f

51 "Tumeaibishwa, kwa maana tumesikia dhihaka. Nyuso zetu zimefunikwa kwa fedheha,

Kwa maana watu wa nchi ya kigeni^{*g} wameshambulia mahali patakatifu pa nyumba ya Yehova."^g

52 "Kwa hiyo tazameni! siku zinakuja," asema Yehova, "Nitakapozikazia fikira sanamu zake za kuchongwa,

Na katika nchi yake yote waliojeruhiwa watalia kwa maumivu."^h

53 "Hata Babiloni akipanda juu mbinguni,ⁱ

Hata akiimarisha ngome zake ndefu,

Watakaomwangamiza wa-

- takuja kutoka kwangu,"^a asema Yehova.
- 54** "Sikilizeni! Kuna kilio kikubwa kutoka Babiloni,^b Sauti ya msiba mkubwa kutoka nchi ya Wakaldayo,^c
- 55** Kwa maana Yehova analiangamiza Babiloni, Atainyamazisha sauti yake kubwa, Na mawimbi yao yatawuma kama maji mengi. Kelele ya sauti yao itasikika.
- 56** Kwa maana mwangamizaji ataishambulia Babiloni;^d Mashujaa wake watakamata,^e Pinde zao zitavunjwavnjwa, Kwa maana Yehova ni Mungu wa kisasi.^f Bila shaka atalipa kisasi.^g
- 57** Nitawaleweshwa wakuu wake na watu wake wenyekheka,^h Magavana wake na watawala wake wasaidizi na mashujaa wake, Nao watalala usingizi wa kudumu, Nao hawataamka kutoka katika usingizi huo,"ⁱ asema Mfalme, ambaye jina lake ni Yehova wa majeshi.
- 58** Yehova wa majeshi anasema hivi: "Ingawa ukuta wa Babiloni ni mpana, utabomolewa kabisa,^j Na ingawa malango yake ni marefu, yatawashwa moto. Watu watafanya kazi ya bure;

SURA YA 51

a Yer 50:10

b Isa 13:6

c Yer 50:22, 23

d Isa 21:2

e Yer 50:36

f Kum 32:35

Zb 94:1

Isa 34:8

Yer 50:29

Ufu 18:5

g Zb 137:8

h Yer 25:27

i Yer 51:39

j Yer 50:15

Yer 51:44

Safu ya 2

a Hab 2:13

b Yer 32:12

Yer 36:4

Yer 45:1

c Isa 13:1, 20

Isa 14:23

Yer 50:3, 39

Yer 51:29, 37

d Ufu 18:21

e Yer 51:58

SURA YA 52

f 2Fa 24:17-20

2Nya 36:11, 12

g 2Fa 23:31

h 2Fa 24:1

2Nya 36:5

Mataifa yatajichosha ili tu kuuchocha moto."^a

59 Hili ndilo neno ambalo nabii Yeremia alimwamuru Seraya mwana wa Neriah^b mwana wa Mahseya ali-poenda na Mfalme Sedekia wa Yuda huko Babiloni katika mwaka wa nne wa utawala wake; Seraya alikuwa msimamizi wa makao. **60** Yeremia aliandika katika kitabu kimoja msiba wote ambao ungepata Babiloni, maneno hayo yote yaliyoandikwa dhidi ya Babiloni. **61** Isitoshe, Yeremia akamwambia Seraya: "Utakapofika Babiloni na kuliona jiji hilo, lazima uyasome kwa sauti kubwa maneno haya yote. **62** Kisha useme, 'Ee Yehova, umesema dhidi ya mahali hapa kwamba pataangamizwa na kubaki bila mkaaji, mwanaadamu au mnyama, na kwamwambia patabaki ukiwa milele.'^c **63** Na utakapomaliza kukisoma kitabu hiki, utakifunga kwenye jiwe na kukitupa katikati ya Mto Efrati. **64** Kisha useme, 'Hivi ndivyo Babiloni atakavyozama naye hatainuka tena kamwe^d kwa sababu ya msiba ambao ninamletea; nao watachoka.'^e

Maneno ya Yeremia yamefikia hapa.

52 Sedekia^f alikuwa na umri wa miaka 21 ali-poanza kutawala, naye alitawala kwa miaka 11 huko Yerusalemu. Mama yake aliitwa Hamutali^g binti ya Yeremia kutoka Libna. **2** Aliendelea kutenda maovu machoni pa Yehova, alitenda mambo yote ambayo Yehoyakimu alitenda.^h **3** Mambo hayo yalitukia Yerusalemu na Yuda kwa

sababu ya hasira ya Yehova, mpaka alipowatupa mbali kutoka machoni pake.^a Na Sedekia akamwasi mfalme wa Babiloni.^b **4** Katika mwaka wa tisa wa utawala wa Sedekia, katika mwezi wa kumi, siku ya kumi ya mwezi huo, Mfalme Nebukadnezah* wa Babiloni alikuja na jeshi lake lote kushambulia Yerusalemu. Walipiga kambi na kujeunga ukuta kulizingira jiji hilo pande zote.^c **5** Nao walilingira jiji hilo mpaka mwaka wa 11 wa utawala wa Mfalme Sedekia.

6 Katika mwezi wa nne, siku ya tisa ya mwezi huo,^d njaa ilikuwa kali sana jijini, na watu waliokuwemo hawakuwa na chakula.^e **7** Mwishowe sehemu ya ukuta wa jiji ikabomolewa, na wanajeshi wote wakakimbia kutoka jijini wakati wa usiku kupitia lango lililokuwa kati ya kuta mbili karibu na bustani ya mfalme, wakati Wakaldayo walipokuwa wakilingira jiji; nao wakafuata njia inayoelekea Araba.^f **8** Lakini jeshi la Wakaldayo likamfuatia mfalme, nalo likamfikia Sedekia^g katika jangwa tambarare la Yeriko, na wanajeshi wake wote wakatawanyika na kumwacha. **9** Kisha wakamkamata mfalme na kumpeleka mpaka kwa mfalme wa Babiloni kule Ribla katika nchi ya Hamathi, naye akamhukumu. **10** Na mfalme wa Babiloni akawachinja wana wa Sedekia huku Sedekia akitazama, na pia akawachinja wakuu wote wa Yuda huko Ribla.

52:4, 12 *Tnn., "Nebukadrezah," njia nyngine ya kuandika jina hili.

SURA YA 52

a Law 26:33
Kum 31:16, 17

b 2Nya 36:11, 13
Eze 17:15

c Kum 28:52
2Fa 25:1, 2
Isa 29:3
Yer 39:1
Eze 4:1, 2
Eze 21:21, 22

d Yer 39:2

e Kum 28:53-57
2Fa 25:3-7
Isa 3:1
Eze 4:16

f Yer 39:4-7

g Yer 24:8
Yer 34:21
Yer 37:17
Yer 38:18

Safu ya 2

a Eze 12:13

b 2Fa 25:8-10

c 1Fa 9:8
2Nya 36:17, 19
Zb 74:8
Zb 79:1
Yer 26:18
Omb 2:7
Eze 24:21

d Yer 39:8

e 2Fa 25:11, 12
Yer 39:9, 10

f 2Fa 25:22

g 1Fa 7:15, 21

h 1Fa 7:27

i 1Fa 7:23
2Nya 4:11-15

j 2Fa 25:13-16
Yer 27:19, 22

11 Kisha mfalme wa Babiloni akampofusha macho Sedekia,^a akamfunga kwa pingu za shaba, akampeleka Babiloni, na kumfunga gerezani mpaka siku aliyokufa.

12 Katika mwezi wa tano, siku ya kumi ya mwezi huo, yaani, mwaka wa 19 wa utawala wa Mfalme Nebukadnezah* wa Babiloni, Nebuzaradani mkuu wa walinzi, aliyekuwa mhudumu wa mfalme wa Babiloni, aliingia Yerusalemu.^b **13** Akateketeza kabisa nyumba ya Yehova,^c nyumba ya* mfalme, na nyumba zote za Yerusalemu; aliteketeza pia kila nyumba kubwa. **14** Na jeshi lote la Wakaldayo lililokuwa pamoja na mkuu wa walinzi lilibomoa kuta zilizozunguka Yerusalemu.^d

15 Nebuzaradani mkuu wa walinzi akawapeleka uhamishoni baadhi ya watu wa hali ya chini na watu wengine waliobaki jijini. Pia aliwachukua watu waliojisalimisha kwa mfalme wa Babiloni na pia mafundi stadi waliobaki.^e **16** Lakini Nebuzaradani mkuu wa walinzi aliwaacha baadhi ya watu maskini kabisa nchini ili watunze mashamba ya mizabibu na kufanya kazi za kulazimishwa.^f

17 Pia Wakaldayo walivunja vipandevipande nguzo za shaba^g za nyumba ya Yehova na magari^h na Bahari ya shaba,ⁱ vitu vilivyokuwa katika nyumba ya Yehova, nao wakapeleka shaba yote hiyo Babiloni.^j **18** Walichukua pia ndoo za kuondolea majivu, sepetu, mikasi ya kukatia tamba

52:13 *Au "jumba la."

za taa, mabakuli,^a vikombe,^b na vyombo vyote vya shaba vilivyotumiwa katika utumishi wa hekaluni. **19** Mkuu wa walinzi alichukua mabeseni,^c vyuetezo, mabakuli, ndoo za kuondolea majivu, vinara vya taa,^d vikombe, na mabakuli yaliyotengenezwa kwa dhahabu na fedha halisi.^e **20** Shaba yote iliyotumiwa kutengeneza zile nguzo mbili, wale ng'ombe dume 12 wa shaba^f waliokuwa chini ya ile Bahari, na yale magari ambayo Mfalme Sulemani alitengeneza kwa ajili ya nyumba ya Yehova, haingeweza kupimwa uzito.

21 Kuhusu nguzo, kila nguzo ilikuwa na kimo cha mikono 18,^{*} na kamba ya kupimia yenye urefu wa mikono 12 ingeweza kuizunguka;^g unene wake ulikuwa upana wa vidole vinne,[#] na ndani ilikuwa wazi.

22 Na kifuniko cha nguzo kilikuwa cha shaba; na urefu wa kila kifuniko ulikuwa mikono mitano;^h na wavu pamoja na makomamanga yote yaliyozunguka kifuniko hicho yalitengenezwa kwa shaba. Nguzo ya pili ilifanana na nguzo ya kwanza, pia yale makomamanga. **23** Kulikuwa na makomamanga 96 kandokando; jumla, kulikuwa na makomamanga 100 kuzunguka ule wavu.ⁱ

24 Mkuu wa walinzi alimchukua pia Seraya mkuu wa makuhani,^j Sefania^k kuhani wa pili, na walinzi watatu wa

52:21 *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14. [#]Upana wa kidole ulilingana na sentimita 1.85 (inchi 0.73). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 52

a 1Fa 7:45

b 2Nya 4:19, 22

c 1Fa 7:38

d 1Fa 7:48, 49

e 2Nya 24:14
2Nya 36:18

f 1Fa 7:23, 25

g 1Fa 7:15-20

h 2Nya 3:15

i 2Nya 3:16
2Nya 4:13j 1Nya 6:14
Ezr 7:1k Yer 21:1, 2
Yer 29:25

Safu ya 2

a 2Fa 25:18-21

b 2Fa 25:6
Yer 52:10c Law 18:25
Law 26:33
Kum 28:36
Isa 24:3
Yer 25:9

d 2Fa 24:12, 14

e Yer 32:1

f Yer 6:9

g 2Fa 24:8
Yer 24:1
Yer 37:1
Mt 1:11

h 2Fa 25:27-30

milango.^a **25** Pia alimchukua kutoka jijini ofisa mmoja wa makao ya mfalme aliyekuwa msimamizi wa wanajeshi, watu saba waliopatikana jijini walioshirikiana kwa ukaribu na mfalme, na pia mwandishi wa mkuu wa jeshi, aliye waandikisha watu jeshini, na wanaume 60 kutoka miongoni mwa watu wa kawaida waliokuwa bado jijini. **26** Nebuzaradani mkuu wa walinzi aliwachukua na kuwapeleka kwa mfalme wa Babiloni kule Ribla. **27** Mfalme wa Babiloni aliwapiga na kuwaangamiza huko Ribla^b katika nchi ya Hamathi. Hivyo watu wa Yuda wakapelekwa uhamishoni kutoka katika nchi yao.^c

28 Hawa ndio watu ambao Nebukadneza* aliwapeleka uhamishoni: katika mwaka wa 7, Wayahudi 3,023.^d

29 Katika mwaka wa 18 wa utawala wa Nebukadneza,^{*e} watu 832 walichukuliwa kutoka Yerusalemu.

30 Katika mwaka wa 23 wa utawala wa Nebukadneza,* Nebuzaradani mkuu wa walinzi aliwapeleka Wayahudi uhamishoni, watu 745.^f

Jumla ya watu 4,600 walipelekwa uhamishoni.

31 Kisha katika mwaka wa 37 tangu Mfalme Yehoyakini^g wa Yuda alipopelekwa uhamishoni, katika mwezi wa 12, siku ya 25 ya mwezi huo, Mfalme Evil-merodaki wa Babiloni, katika mwaka alioanza kutawala, alimwachilia huru Mfalme Yehoyakini wa Yuda na kumtoa gerezeni.^h **32** Alizungumza naye kwa fadhili

52:28-30 *Tnn., "Nebukadreza," njia nyingine ya kuandika jina hili.

na kukikweza kiti chake cha ufalme juu zaidi kuliko viti vya wafalme wengine waliokuwa pamoja naye Babiloni. **33** Basi Yehoyakini akavua mavazi yake ya gereza-ni, na sikuzote za maisha yake

alikuwa akila kwenye meza ya mfalme. **34** Naye alipe-wa chakula kwa ukawaida kutoka kwa mfalme wa Babiloni, siku baada ya siku, mpa-ka siku aliyokufa, siku zote za maisha yake.

MAOMBOLEZO

YALIYOMO

- | | |
|--|---|
| <p>1 Jiji la Yerusalemu lafananishwa na mjane
Limebaki ukiwa na kuachwa (1)
Dhambi nzito sana za Sayuni (8, 9)
Sayuni lakataliwa na Mungu (12-15)
Hakuna wa kulifariji Sayuni (17)</p> <p>2 Hasira ya Yehova dhidi ya Yerusalemu Hakulihurumia (2)
Yehova ni kama adui yake (5)
Machozi yamwagwa kwa ajili ya Sayuni (11-13)
Wapita njia walidharau jiji lililokuwa maridadi awali (15)
Maadui washangilia kuanguka kwa Sayuni (17)</p> <p>3 Yeremia aeleza hisia na matumaini yake
"Nitaonyesha mtazamo wa kungojea" (21)
Rehema za Mungu ni mpya kila asubuhi (22, 23)</p> | <p>Mungu ni mwema kwa wale wanaomtumaini (25)
Ni jambo jema kwa vijana kubeba nira (27)
Mungu aziba kwa wingu njia ya kumkaribia (43, 44)</p> <p>4 Matokeo mabaya ya kuzingirwa kwa Yerusalemu
Ukosefu wa chakula (4, 5, 9)
Wanawake wawachemsha watoto wao wenyewe (10)
Yehova amemwaga hasira yake (11)</p> <p>5 Watu wasali warudishwe
'Kumbuka yale ambayo yametupata' (1)
'Ole wetu; tumetenda dhambi' (16)
'Turudishe, Ee Yehova' (21)
"Zifanye siku zetu ziwe mpya" (21)</p> |
|--|---|

ℵ [Aleph]*

1 Lo! Jiji lililokuwa limejaa watu^a sasa limebaki ukiwa!

Limekuwa kama mjane, jiji lililokuwa na watu wengi miongoni mwa mataifa!^b

1:1 *Sura ya 1-4 ni nyimbo za maombolezo zilizoandikwa kwa kufuata alfabeti za Kiebrania au mpangilio wa kishairi.

SURA YA 1

a Zb 122:3, 4

b 1Fa 4:20

Safu ya 2

a Kum 28:15, 48
2Fa 25:11, 12

b Omb 1:16

Jiji lililokuwa binti ya mfalme kati ya mikoa* limefanywa kuwa mtu-mwa!^a

Ⓛ [Beth]

2 Binti huyo analia sana usiku,^b na machozi yake yamefunika mashavu yake.

Miongoni mwa wapenzi

1:1 *Au "wilaya ya utawala."

wake wote hakuna yeyote wa kumfariji.^a

Marafiki zake wote wamemsaliti;^b wamekuwa maadui wake.

‡ [Gime]

- 3 Yuda amepoleka uhamishoni^c kwa mateso na utumwa wa kikatili.^d

Ni lazima akae miongoni mwa mataifa;^e hana mahali pa kupumzika.

Wote waliokuwa wakimtesa wamemkabili katika mateso yake.

‡ [Daleth]

- 4 Barabara zinazoeleka Sayuni zinaomboleza, kwa sababu hakuna yeyote anayekuwa kwenye she-rehe.^f

Malango yake yote yamebaki ukiwa;^g makuhani wake wanalia kwa uchungu.

Mabikira* wake wanaomboleza, naye analia kwa maumivu makali.

‡ [He]

- 5 Wapinzani wake sasa ni mabwana wakubwa wake; maadui wake hawajali.^h

Kwa maana Yehova amemletea huzuni kwa sababu ya dhambi zake nyingi.ⁱ

Adui amewapeleka watoto wake utekwani.^j

‡ [Waw]

- 6 Fahari yote ya binti ya Sayuni imetoweka.^k
Wakuu wake ni kama paa dume waliokosa malisho, Nao wanatembea kwa uchovu mbele ya yule anayewafuatia.

SURA YA 1

a Yer 4:30
Eze 16:37

b Yer 30:14

c Law 26:33
2Fa 24:14, 15
2Fa 25:21
Yer 39:9
Yer 52:27

d Yer 17:4

e Kum 28:64

f Amo 8:10

g Isa 3:26

h Zek 1:15

i 2Nya 36:15, 16
Ne 9:33
Da 9:7, 16

j Yer 39:9
Yer 52:30

k Eze 24:21

Safu ya 2

a 1Fa 10:27

b Yer 52:4

c Zb 137:7
Omb 2:16

d Isa 1:4
Isa 59:2
Eze 22:4

e Yer 13:22
Eze 23:29

f Yer 4:31

g Yer 8:7

h Yer 50:29

i Yer 52:17, 19
Da 1:1, 2

j 2Nya 36:17, 18
Zb 74:7
Yer 52:13

† [Zayin]

- 7 Katika siku za mateso yake na za kukosa makao, Yerusalemu hukumbuka

Vitu vyote vyenye thamani vilivyokuwa vyake siku za zamani za kale.^a

Watu wake walipotiwa mikononi mwa adui, naye hakuwa na msaidizi,^b

Maadui walimwona na kumcheka* alipoanguka.^c

‡ [Heth]

- 8 Yerusalemu ametenda dhambi nzito sana.^d
Ndiyo sababu amekuwa kitu kinachochukiza sana.

Wote waliokuwa wakimheshimu sasa wanamtembea kama kitu kinachodharauliwa, kwa maana wameuona uchi wake.^e

Yeye mwenyewe analia kwa maumivu^f na kujificha kwa aibu.

‡ [Teth]

- 9 Uchafu wake umo ndani ya mavazi yake.
Hakufikiria wakati wake ujao.^g

Alianguka kwa njia ya kushangaza; hana yeyote wa kumfariji.

Ee Yehova, yaangalie mateso yangu, kwa sababu adui amejitukuza.^h

† [Yod]

- 10 Adui amechukua hazina zake zote.ⁱ

Kwa maana ameona* mataifa yakiingia mahali pake patakatifu,^j

Watu ulioamuru wasiingie katika kutaniko lako.

1:7 *Au "kumdhihaki." 1:10 *Yaani, watu wa Yerusalemu.

☞ [Kaph]

- 11 Watu wake wote wanalia kwa chungu; wanatafuta mkate.^a

Wamewapa vitu vyao vyenye thamani ili wapate kitu cha kula, angalau waendeleo kuishi.*

Tazama, Ee Yehova, uone kwamba nimekuwa kama mwanamke asiyeftaa kitu.[#]

↳ [Lamed]

- 12 Enyi nyote mnaopita njiani, mateso yangu kwenu si kitu?

Tazameni mwone!

Je, kuna maumivu kama maumivu niliyoletewa, Ambayo Yehova aliniletea katika siku ya hasira yake kali?^b

☞ [Mem]

- 13 Kutoka juu sana ameusha moto mifupani mwangu,^c naye anauiisha kila mfupa.

Ametandaza wavu wa kunasa miguu yangu; amenilazimisha nirudi nyuma.

Amenifanya kuwa mwanaamke aliye ukiwa.

Mchana kutwa mimi ni mgonjwa.

⌋ [Nun]

- 14 Dhambi zangu zimefungwa kama nira, mkono wake umezifunga pamoja.

Zimewekwa shingoni mwangu, nami nimeishiwa na nguvu.

Yehova amenitia mikononi mwa watu ambao siwezi kuwapinga.^d

1:11 *Au "wahuishe nafsi." #Jiji la Yerusalemu linafananishwa na mwanamke.

SURA YA 1

a Yer 38:9
Yer 52:6
Omb 2:12
Omb 4:4

b Yer 21:7

c Zb 102:3

d Law 26:37
Eze 11:9

Safu ya 2

a 2Fa 24:14, 15

b 2Nya 36:17

c Ufu 14:19
Ufu 19:15

d Yer 31:15

e Yer 4:31

f Kum 28:49
2Fa 24:1, 2
2Fa 25:1

g Omb 1:8

h Ne 9:33
Da 9:7

i 1Sa 12:14, 15

j Kum 28:32

k Yer 30:14

☞ [Samekh]

- 15 Yehova amewatupa pembeni watu wote wenye nguvu kati yangu.^a

Ameokusanya umati wa watu dhidi yangu ili kuwaponda vijana wangu wa kiume.^b

Yehova amemkanyaga binti bikira wa Yuda katika shinikizo la divai.^c

☞ [Ayin]

- 16 Ninalia kwa sababu ya mambo haya;^d macho yangu yanatiririka machozi.

Kwa maana yeyote ambaye angenifariji au kuniburudisha yuko mbali sana nami.

Wanangu wamebaki ukiwa, kwa maana adui ameshinda.

☞ [Pe]

- 17 Sayuni amenyoosha mikonoyake;^e hana wa kumfariji.

Yehova amewaagiza madi wote wanaomzunguka Yakobo wamshambulie.^f

Yerusalemu limekuwa kitu cha kuchukiza sana kwao.^g

☞ [Tsade]

- 18 Yehova ni mwadilifu,^h kwa kuwa nimeasi amri zake.^{*i}

Sikilizeni, enyi mataifa yote, mwone maumivu yangu.

Mabikira[#] wangu na vijana wangu wa kiume wamepeleka utekwani.^j

☞ [Qoph]

- 19 Nimewaita wapenzi wangu, lakini wamenisaliti.^k

1:18 *Tnn., "nimekiasi kinywa chake."
#Au "Wanawali."

Makuhani wangu na wazee wangu wameangamia jijini,

Walipokuwa wakitafuta chakula ili waendelee kuishi.*^a

↯ [Resh]

- 20 Tazama, Ee Yehova, kwa maana ninateseka sana. Matumbo yangu yanasukasuka.

Moyo wangu umepinduka ndani yangu, kwa maana nimekuwa mwasi kabisa.^b

Nje, upanga unaangamiza;^c ndani ya nyumba, ni kama kifo.

↯ [Shin]

- 21 Watu wamesikia kilio changu cha uchungu; hakuna yeyote wa kunifariji. Maadui wangu wote wamesikia kuhusu msiba wangu.^d

Wanashangilia, kwa sababu uliuleta.

Lakini utaleta siku uliyotangaza,^e wakati huo watakuwa kama mimi.^f

↯ [Taw]

- 22 Uovu wao wote na uje mbele zako, na uwatese vikali,^g Kama tu ulivyonitesa vikali kwa sababu ya dhambi zangu zote. Kwa maana vilio vyangu vya uchungu ni vingi, na moyo wangu ni mgonjwa.

↯ [Aleph]

- 2 Jinsi Yehova alivyomfunika binti ya Sayuni katika wingu la hasira yake! Ameutupa chini urembo wa Israeli kutoka mbinguni mpaka duniani.^h

SURA YA 1

a 2Fa 25:3
Yer 38:9

b Zb 107:11
Isa 1:2
Isa 63:10

c Kum 32:25
Yer 15:2

d Eze 25:6, 7
Oba 12

e Isa 13:19
Yer 25:12-14
Yoe 3:19

f Zb 137:8, 9
Isa 51:22, 23

g Yer 51:35

SURA YA 2

h Omb 2:15

Safu ya 2

a 1Nya 28:2
Zb 132:7
Isa 60:13

b Kum 28:52
Mik 5:11

c Eze 21:26, 27

d Isa 39:7
Isa 43:28

e Zb 74:10, 11

f Kum 32:22
Isa 42:25
Yer 7:20

g Kum 28:63
Isa 63:10
Yer 21:5

h 2Fa 25:21

i Yer 4:4

j Yer 10:20

k Yer 30:14

Hajakumbuka kiti cha miguu yake^a katika siku ya hasira yake.

↯ [Beth]

- 2 Yehova ameyameza makao yote ya Yakobo bila huruma. Katika hasira yake amebomoa ngome za binti ya Yuda.^b Ameushusha chini ardhini na kuuchafua ufalme^c na wakuu wake.^d

↯ [Gimef]

- 3 Kwa hasira kali amezikata nguvu zote za* Israeli. Aliuondoa mkono wake wa kuume adui alipokaribia,^e

Na katika Yakobo aliendelea kuwaka kama moto ulioteketeza kila kitu kilicho karibu.^f

↯ [Daleth]

- 4 Ameukunja* upinde wake kama adui; mkono wake wa kuume uko tayari kama adui;^g Aliendelea kuwaua wote wanaotamanika machoni.^h Naye aliimwaga ghadhabu yake kama motoⁱ katika hema la binti ya Sayuni.^j

↯ [He]

- 5 Yehova amekuwa kama adui;^k Ameimeza Israeli. Ameimeza minara yake yote; Ameziharibu ngome zake zote. Na katika binti ya Yuda anafanya maombolezo na kilio kiwe kingi.

2:3 *Tnn., "ameikata kila pembe ya."

2:4 *Tnn., "Ameukanyaga."

† [Waw]

- 6 Anakitendea kwa ukatili kibanda chake,^a kama kibanda kilicho katika bustani.

Amekomesha* sherehe yake.^b

Yehova amesababisha sherehe na sabato zisahauliwe Sayuni,

Na kwa ghadhabu yake kali hambahimu mfalme na kuhani.^c

† [Zayin]

- 7 Yehova amekataa madhabu yake;

Amedharau mahali pake patakatifu.^d

Amesalimisha kuta za minara yake yenye ngome mikononi mwa adui.^e

Wameinua sauti yao ndani ya nyumba ya Yehova,^f kama inavyokuwa siku ya sherehe.

† [Heth]

- 8 Yehova amezimia kuuharibu ukuta wa binti ya Sayuni.^g

Ameinyoosha kamba ya kupimia.^h

Hajauzia mkono wake usilete maangamizi.*

Naye husababisha maboma na kuta ziomboleze. Zote pamoja zimedhoofishwa.

‡ [Teth]

- 9 Malango yake yamezama chini ardhini.ⁱ

Ameyaharibu na kuyavunja makomeo yake.

Mfalme wake na wakuu wake wako miongoni mwa mataifa.^j

SURA YA 2

a 2Fa 25:8, 9
2Nya 36:19
Isa 63:18
Isa 64:11

b Omb 1:4

c Yer 52:24, 27

d Law 26:31
Yer 26:6
Yer 52:12, 13
Eze 24:21
Mik 3:12

e 2Nya 36:19

f Zb 74:4

g 2Fa 25:10
Yer 39:8

h 2Fa 21:13
Isa 28:17

i Ne 1:3
Yer 14:2

j Kum 28:15, 36
2Fa 24:15
2Fa 25:7
Omb 4:20
Eze 12:13
Da 1:3, 6

Safu ya 2

a Zb 74:9
Yer 23:16
Eze 7:26

b Isa 3:26

c Yer 6:26
Eze 7:18

d Omb 3:48

e Yer 14:17

f Yer 11:22
Omb 2:19
Omb 4:4

g Kum 28:49, 51
2Fa 25:3
Isa 3:1
Yer 18:21

Hakuna sheria;* hata manabii wake hawapati maono kutoka kwa Yehova.^a

† [Yod]

- 10 Wazee wa binti ya Sayuni wanaketi ardhini wakiwa kimya.^b

Wanarusha mavumbi vichwani mwao na kuvaa nguo za magunia.^c

Mabikira wa Yerusalemu wameinamisha vichwa vyao mpaka ardhini.

‡ [Kaph]

- 11 Macho yangu yamechoka kabisa kwa sababu ya kumwaga machozi.^d

Matumbo yangu yanasukasuka.

Ini langu limemwagika ardhini, kwa sababu ya kuanguka kwa binti ya* watu wangu,^e

Kwa sababu ya watoto wadogo na watoto wanaonyonya wanaozimia kwenye viwanja vya mji.^f

‡ [Lamed]

- 12 Wanaendelea kuwauliza mama zao, "Iko wapi nafaka na divai?"^g

Wanapozimia kama mtu aliyejeruhiwa katika viwanja vya mji,

Huku uhai wao ukitoka polepole wakiwa mikononi mwa mama zao.

‡ [Mem]

- 13 Ninaweza kutumia nini kama ushahidi, Au ninaweza kukufanisha na nini, Ee binti ya Yerusalemu?

2:9 *Au "mafundisho." 2:11 *Mfano wa kishairi ambao huenda unaonyesha huruma au sikitiko.

2:6 *Au "Ameharibu." 2:8 *Tnn., "usi-meze."

Ninaweza kukulinganisha
na nini, ili nikufariji, Ee
bikira binti ya Sayuni?

Kwa maana jeraha lako*
ni kubwa kama bahari.^a
Ni nani anayeweza kuku-
ponya?^b

‡ [Nun]

- 14** Maono ambayo manabii
wako waliona kwa ajili
yako yalikuwa ya uwo-
ngo na yasiyofaa kitu,^c
Nao hawakufunua kosa
lako ili kuzuia usipele-
kwe utekwani,^d
Bali waliendelea kukupa
maono yenye ujumbe
wa uwongo na unaopo-
tosha.^e

⊕ [Samekh]

- 15** Wote wanaopita baraba-
rani wanakupigia makofi
kwa dharau.^f
Wanapiga mluzi kwa mshang-
ngao^g na kumtikisia vi-
chwa vyao binti ya Yeru-
salemu, wakisema:
“Je, hili ndilo jiji walilose-
ma hivi kulihusu: ‘Lina
urembo mkamilifu, ni
shangwe ya dunia
yote?’”^h

⊞ [Pe]

- 16** Maadui wako wote wame-
fungua kinywa chao dhi-
di yako.
Wanapiga mluzi na kusaga
meno yao wakisema:
“Tumemmeza.ⁱ
Hii ndiyo siku tuliyokuwa
tukiingojea!^j Imefika,
nasi tumeiona!”^k

‡ [Ayin]

- 17** Yehova ametenda aliloku-
sudia,^l ametekeleza neno
lake,^m

2:13 *Au “jeraha lako la kuvunjika.”

SURA YA 2

a Yer 14:17
Da 9:12

b Yer 30:12

c Yer 2:8
Yer 27:14
Eze 13:2, 3

d Yer 23:14

e Yer 23:32
Yer 27:9
Mik 3:5
Sef 3:4

f Eze 25:2, 6

g 1Fa 9:8
Yer 25:9

h Zb 48:2
Eze 16:14

i Yer 51:34

j Mik 4:11

k Oba 13

l Yer 18:11
Mik 2:3

m 2Fa 23:27

Safu ya 2

a Law 26:14, 17
Kum 28:15

b Eze 5:11

c Isa 51:20
Omb 4:9
Eze 5:16

d Law 26:29
Kum 28:53
Yer 19:9
Omb 4:10
Eze 5:10

e Eze 9:6, 7

Aliloamuru zamani za
kale.^a

Amebomoa bila huruma.^b
Amemruhusu adui asha-
ngilie msiba wako; ame-
zikweza nguvu za* wapi-
nzani wako.

‡ [Tsade]

- 18** Moyo wao unamlilia Yeho-
va kwa sauti, Ee ukuta
wa binti ya Sayuni.
Machizi na yatiririke
kama mto mchana na
usiku.
Usipumzike, macho yako
yasiache kulia.*

‡ [Qoph]

- 19** Inuka! Lia kwa sauti wa-
kati wa usiku, mwanzoni
mwa makesha ya usiku.
Umwage moyo wako kama
maji mbele za uso wa Ye-
hova.
Mwinulie mikono yako kwa
ajili ya uhai wa* watoto
wako,
Wanaozimia kwenye kila
pembe ya barabara kwa
sababu ya njaa kali.^c

‡ [Resh]

- 20** Tazama, Ee Yehova,
umwone yule uliye-
mtesa vikali.
Je, wanawake wanapaswa
kuendelea kula uzao wao
wenyewe, watoto wao
wenyewe waliokomaa,^d
Au, je, makuhani na ma-
nabii wanapaswa kuua-
wa mahali patakatifu pa
Yehova?^e

‡ [Shin]

- 21** Mvulana na mwanamume
mzee wamelala chini

2:17 *Tnn., “ameikweza pembe ya.”
2:18 *Tnn., “binti ya jicho lako asipu-
mzike.” 2:19 *Au “nafsi za.”

barabarani wakiwa wamekufa.^a

Mabikira* wangu na vijana wangu wa kiume wameuawa kwa upanga.^b

Umeua katika siku ya hasira yako; umechinja bila huruma.^c

⌈ [Taw]

22 Unakusanya vitisho kuto-ka kila upande kana kwamba ni siku ya sherehe.^d

Katika siku ya ghadhabu ya Yehova, hakuna yeyote aliyeponyoka wala kuokoka;^e

Wale niliowazaa* na kuwalea, adui yangu aliwaa-ngamiza kabisa.^f

⌘ [Aleph]

3 Mimi ndiye mwanamume aliyepata mateso kwa sababu ya fimbo ya ghadhabu yake.

2 Amenifukuza, naye hunifanya nitembee gizani, si nuruni.^g

3 Kwa kweli, yeye huniadhibu tena na tena kwa mkono wake mchana kutwa.^h

⌋ [Beth]

4 Ameudhoofisha mwili wangu na ngozi yangu;

Ameivunja mifupa yangu.

5 Amenizingira; amenizungushia sumuⁱ kali na taabu.

6 Amenilazimisha niketi katika sehemu zenye giza, kama watu waliokufa za mani za kale.

⌋ [Gimel]

7 Amenizungushia ukuta, hivi kwamba siwezi kutoroka;

2:21 *Au "Wanawali." 2:22 *Au "nilio-wazaa wakiwa na afya."

SURA YA 2

a Kum 28:49, 50
2Nya 36:17

b Yer 9:21
Yer 18:21

c Yer 13:14
Yer 21:7
Omb 3:43
Eze 5:11
Eze 9:6

d Kum 16:16

e Sef 1:18

f Kum 28:18

SURA YA 3

g Kum 28:15, 29
Yer 13:16

h Isa 63:10

i Yer 8:14
Yer 9:15
Omb 3:19

Safu ya 2

a Yer 39:7

b Zb 80:4
Zb 102:2
Isa 1:15
Mik 3:4

c Isa 63:17

d Ayu 38:39, 40
Ho 5:14
Amo 5:18, 19

e Yer 6:8
Yer 32:43

f Yer 9:15
Yer 23:15

g Zb 102:9
Yer 6:26

Amenifunga kwa pingunzito za shaba.^a

8 Na ninapolilia sana msaa-da, yeye hukataa* sala yangu.^b

9 Ameviziba vijia vyangu kwa mawe yaliyocho-
ngwa;

Amezifanya barabara zangu zipinde.^c

⌈ [Dalath]

10 Anangojea kunivizia kama dubu, kama simba aliye mafichoni.^d

11 Amenisukuma kutoka kwenye vijia na kunirarua vipandevipande;*

Amenifanya nibaki ukiwa.^e

12 Ameukunja* upinde wake, naye hunifanya niwe shabaha ya mshale wake.

⌈ [He]

13 Amezichoma figo zangu kwa mishale ya* podo lake.

14 Nimekuwa kichekesho kwa mataifa yote, kichwa cha wimbo wao mchana kutwa.

15 Amenijaza mambo machungu na kunikoleza kwa pakanga.^f

⌈ [Waw]

16 Huyavunja meno yangu kwa changarawe;

Hunifanya nijikunyate kwa woga katika majivu.^g

17 Unaninyima amani; nimesahau lililo jema.

18 Kwa hiyo ninasema: "Fahari yangu imetoweka, na pia matarajio yangu kwa Yehova."

3:8 *Au "huizua; huifungia nje." 3:11 *Au labda, "ananiacha kama shamba ambalo halijapandwa mbegu." 3:12 *Tnn., "Ameukanyaga." 3:13 *Tnn., "wana wa."

† [Zayin]

- 19 Kumbuka mateso yangu na hali yangu ya kukosa makao,^a pakanga na sumu kali.^b
- 20 Kwa hakika utakumbuka na kuinama juu yangu.^c
- 21 Ninakumbuka hili moyoni mwangu; ndiyo sababu nitaonyesha mtazamo wa kungojea.^d
- 22 Hatujaangamia kwa saba-bu ya upendo mshikamanifu wa Yehova,^e
Kwa maana rehema zake hazikomi kamwe.^f
- 23 Ni mpya kila asubuhi;^g uaminifu wako ni mwingi sana.^h
- 24 Nimesema, * “Yehova ni fungu languⁱ ndiyo sababu nitaonyesha mtazamo wa kumngojea yeye.”^j

‡ [Teth]

- 25 Yehova ni mwema kwa yule anayemtumaini,^k kwa mtu anayeendelea kumtafuta.^l
- 26 Ni jambo jema kuungojea kimyakimya^{*m} wokovu wa Yehova.ⁿ
- 27 Ni jambo jema kwa mwana-mume kubeba nira wakati wa ujana.^o

* [Yod]

- 28 Acha akae peke yake na kunyamaza Mungu ana-poiweka juu yake.^p
- 29 Acha atie kinywa chake mavumbini;^q huenda ika-wa bado kuna tumaini.^r
- 30 Acha ampe shavu lake yule anayempiga; acha atukanwe vya kutosha.

3:24 *Au “Nafsi yangu inasema.” 3:26

*Au “kuungojea kwa subira.”

SURA YA 3

a Ne 9:32
Zb 137:1
b Yer 9:15
Omb 3:5
c Zb 113:5-7
d Zb 130:6-8
Mik 7:7
e Ezz 9:8
f Ne 9:31
Yer 30:11
Mik 7:18
g Zb 30:5
h Kum 32:4
Zb 36:5
i Zb 16:5
Zb 73:26
Zb 142:5
j Zb 130:6-8
k Zb 25:3
Zb 130:5
Isa 25:9
Isa 30:18
Mik 7:7
l 1Nya 28:9
Isa 26:9
Sef 2:3
m Zb 37:7
n Zb 116:6
o Zb 119:71
p Zb 39:8, 9
Omb 3:39
q Eze 16:63
r Yoe 2:12-14

Safu ya 2

a Yer 3:12
Yer 31:37
Yer 32:40
Mik 7:18
b Zb 30:5
Zb 103:9, 11
Isa 54:7
Yer 31:20
c Isa 55:7
Eze 33:11
2Pe 3:9
d Zb 102:19, 20
e Zb 12:5
Met 17:15
f Zb 103:10
Mik 7:9
g Hag 1:5
h Kum 4:30
Isa 55:7
Yoe 2:13
i Kum 4:29
2Nya 7:14
2Nya 34:27
j Ne 9:26
k 2Fa 24:3, 4
Da 9:5, 12

‡ [Kaph]

- 31 Kwa maana Yehova hata-tutupa mbali milele.^a
- 32 Ingawa amesababisha hu-zuni, ataonyesha pia re-hema kulingana na upe-ndo wake mwingi sana mshikamanifu.^b
- 33 Kwa maana moyo wake haupendi kuwatesa au kuwahuzunisha wana-damu.^c
- 34 Kuwaponda chini ya nya-yo wafungwa wote wa dunia,^d
- 35 Kumnyima mtu haki yake mbele za Aliye Juu Zaidi,^e
- 36 Kumlaghai mtu katika kesi yake
—Yehova havumilii mambo kama hayo.

‡ [Mem]

- 37 Kwa hiyo basi, ni nani anayeweza kusema na jambo likatendeka Yeho-va asipoamuru?
- 38 Kutoka katika kinywa cha Aliye Juu Zaidi, Mambo mabaya na mema hayatoki pamoja.
- 39 Kwa nini mtu aliye hai ala-lamike kuhusu matokeo ya dhambi yake?^f

‡ [Nun]

- 40 Acheni tuzikague na ku-zichunguza kwa makini njia zetu,^g na acheni tu-mrudie Yehova.^h
- 41 Acheni tuinue mioyo yetu pamoja na mikono yetu kwa Mungu mbi-nguni!ⁱ
- 42 “Tumetenda dhambi na kuasi,^j nawe hujatusa-mehe.^k

◊ [Samekh]

43 Kwa hasira umeziba njia tusikukaribie;^a

Umetufuatia na kutuua bila huruma.^b

44 Umeziba kwa wingu njia ya kukukaribia, ili sala yetu isipenye.^c

45 Unatufanya kuwa takataka na uchafu miongoni mwa mataifa.”

▣ [Pe]

46 Maadui wetu wote wanafungua vinywa vyao dhidi yetu.^d

47 Hofu na mitego vimekuwa fungu letu,^e ukiwa na maangamizi.^f

48 Vijito vya maji vinatiririka kutoka katika macho yangu kwa sababu ya maangamizi ya binti ya watu wangu.^g

⋈ [Ayin]

49 Macho yangu yanamwaga machozi bila kikomo, hayapumziki,^h

50 Mpaka Yehova atakapoangalia na kuona kutoka mbinguni.ⁱ

51 Macho yangu yameniletea huzuni kwa sababu ya mabinti wote wa jiji langu.^j

⋈ [Tsade]

52 Maadui wangu wameniwinda sana kama ndege bila sababu.

53 Wameunyamazisha uhai wangu shimoni; waliendelea kunitupia mawe.

54 Maji yalitiririka juu ya kichwa changu, nami nika sema: “Nimekwisha!”

◊ [Qoph]

55 Nililiita jina lako kwa sauti, Ee Yehova, kutoka chini shimoni.^k

SURA YA 3

a Met 15:8

b Kum 4:26
Omb 2:2
Eze 9:10

c Zb 80:4
Met 15:29
Met 28:9
Isa 1:15
Mik 3:4
Zek 7:13

d Omb 2:16

e Kum 28:66, 67

f Isa 51:19
Yer 4:6

g Yer 9:1

h Yer 14:17
Omb 1:16

i Zb 80:14
Zb 102:19-21
Isa 63:15

j Yer 11:22

k Zb 130:1
Yon 2:1, 2

Safu ya 2

a Yer 50:34

b Yer 51:36, 37

c Zb 74:18

SURA YA 4

d 1Fa 6:22

e 1Fa 5:17
1Fa 7:9-12

56 Isikie sauti yangu; usizibe sikio lako ninapolilia msaada, ninapoomba kitulizo.

57 Ulinikaribia siku niliyokuita. Ulisema: “Usiogope.”

◊ [Resh]

58 Umenitetea, * Ee Yehova, umeukomboa uhai wangu.^a

59 Umeona, Ee Yehova, uovu niliotendewa; tafadhali nitendee haki.^b

60 Umeona kisasi chao choote, njama zao zote walizopanga dhidi yangu.

⋈ [Sin] au [Shin]

61 Umesikia dhihaka zao, Ee Yehova, njama zao zote walizopanga dhidi yangu,^c

62 Midomo ya wapinzani wangu na mambo wanayong'ona dhidi yangu mchana kutwa.

63 Watazame; wananidhahaki kwa nyimbo zao wakiwa wameketi au wamesimama!

◊ [Taw]

64 Utawalipa, Ee Yehova, kuilingana na matendo yao.

65 Utaifanya mioyo yao kuwa migumu, kama laana kwao.

66 Utawafuatia kwa hasira yako na kuwaangamiza chini ya mbingu zako, Ee Yehova.

⋈ [Aleph]

4 Jinsi dhahabu inayong'aa ilivyopoteza mng'ao wake, dhahabu bora!^d Jinsi mawe matakatifu^e

3:58 *Au “Umezitetea kesi za nafsi yangu.”

yalivyotapakaa kwenye
kila pembe ya barabara!^a

‡ [Beth]

- 2 Na wana wa Sayuni wenye
thamani, ambao walipi-
mwa kwa uzito wa* dha-
habu safi,

Sasa wanaonwa kuwa
kama magudulia ya
udongo,

Kazi ya mikono ya mfi-
nyanzi!

‡ [Gime]

- 3 Hata mbwamwitu huwapa
watoto wao matiti wa-
nyonye,

Lakini binti ya watu wangu
amekuwa mkatili,^b kama
mbuni nyikani.^c

‡ [Daleth]

- 4 Ulimi wa mtoto anayenyo-
nya hushikamana na
kaakaa lake kwa sababu
ya kiu.

Watoto wadogo wanao-
mbaomba mikate,^d lakini
hakuna anayewapa.^e

‡ [He]

- 5 Wale waliokuwa wakila
vyakula vitamu wanalala
barabarani kwa sababu
ya njaa kali.^f

Wale waliotelewa wakivaa
mavazi mekundu^g wame-
kumbatia marundo ya
majivu.

‡ [Waw]

- 6 Adhabu* ya binti ya watu
wangu ni kubwa kuliko
adhabu iliyotolewa kwa
sababu ya dhambi ya So-
doma,^h

Lililopinduliwa haraka, na
hakukuwa na mtu wa ku-
lisaidia.ⁱ

4:2 *Au "waliokuwa na thamani kama."
4:6 *Tnn., "Dhambi." #Tnn., "bila mko-
no wa kulisaidia."

SURA YA 4

a Yer 52:12, 13

b Law 26:29
Kum 28:53-57
Yer 19:9
Omb 4:10

c Ayu 39:14-16

d Omb 1:11
Omb 2:11, 12

e Yer 52:6

f Amo 6:4, 7

g Yer 6:2, 26

h Eze 16:48

i Mwa 19:24, 25
Da 9:12

Safu ya 2

a Hes 6:2

b Zb 102:5

c Yer 29:17
Yer 38:2

d Law 26:29
Omb 2:20
Omb 4:3

e Kum 28:54-57

f Yer 6:11
Yer 7:20
Eze 22:31

g Kum 32:22
2Fa 25:9, 10

† [Zayin]

- 7 Wanadhiri wake^a waliku-
wa safi kuliko theluji,
weupe kuliko maziwa.

Walikuwa wekundu kuliko
marijani; walikuwa kama
vito vya yakuti vilivyo-
ng'arishwa.

‡ [Heth]

- 8 Wamekuwa weusi kuliko
masizi;*

Hawatambuliwi baraba-
rani.

Ngozi yao imenyauka juu
ya mifupa yao;^b imekuwa
kama ukuni uliokauka.

‡ [Teth]

- 9 Waliouawa kwa upanga ni
afadhali kuliko walioku-
fa kwa njaa kali,^c

Wale wanaokonda, wanao-
chomwa kana kwamba
kwa upanga kwa sababu
ya kukosa chakula kuto-
ka shambani.

* [Yod]

- 10 Mikono ya wanawake we-
nye huruma imewache-
msha watoto wao wenye-
we.^d

Wamekuwa chakula chao
cha maombolezo wakati
wa kuangamia kwa binti
ya watu wangu.^e

‡ [Kaph]

- 11 Yehova ameonyesha gha-
dhabu yake;

Amemwaga hasira yake
kali.^f

Anawasha moto Sayuni
naoteketeza misingi
yake.^g

‡ [Lamed]

- 12 Wafalme wa dunia na wa-
kaazi wote wa ardhi ina-
yozaa hawakuamini

4:8 *Tnn., "weusi."

Kwamba mpinzani na adui wangeingia katika malango ya Yerusalemu.^a

ⲙ [Mem]

- 13** Hilo lilitokea kwa sababu ya dhambi za manabii wake, makosa ya makuhani wake,^b

Waliomwaga damu ya waa-dilifu waliokuwa katika jiji hilo.^c

ⲓ [Nun]

- 14** Wametangatanga kama vipofu^d barabarani.

Wamechafuliwa na damu,^e

Hivi kwamba hakuna yeyote anayeweza kuyagusa mavazi yao.

ⲛ [Samekh]

- 15** “Nendeni zenu! Wachafu!” watu wanawaambia kwa sauti. “Nendeni zenu! Nendeni zenu! Msituguse!”

Kwa maana hawana makao, nao wanatangatanga.

Miongoni mwa mataifa watu wamesema: “Hawa-zezi kukaa hapa pamoja nasi.”^{*f}

ⲛ [Pe]

- 16** Uso wa Yehova umewatawanya;^g

Hatawaonyesha tena kibali chake.

Watu hawatawaheshimu makuhani,^h hawatawatendea wazee kwa fadhili.”ⁱ

ⲙ [Ayin]

- 17** Hata sasa macho yetu yamechoka kabisa tukitarajia kupata msaada bila mafanikio.^j

SURA YA 4

a Kum 29:24
1Fa 9:8

b Yer 5:31
Yer 14:14
Mik 3:11
Sef 3:4

c Yer 26:8
Mt 23:31
Mdo 7:52

d Kum 28:28
Sef 1:17

e Isa 1:15
Yer 2:34

f Kum 28:25, 65

g Law 26:33
Kum 28:64
Yer 24:9

h 2Fa 25:18, 21

i Omb 5:12
Eze 9:6

j Omb 1:19

Safu ya 2

a Yer 37:7
Eze 29:6

b 2Fa 25:5
Omb 3:52

c Kum 28:49, 50
Isa 5:26
Yer 4:13
Hab 1:8

d Yer 37:1

e 2Fa 25:5, 6
Yer 39:5

f Zb 137:7
Oba 12

g Yer 25:17, 20
Oba 16

h Yer 49:10, 12

i Law 26:44
Isa 52:1
Isa 60:18

j Isa 34:5
Eze 25:13
Eze 35:15
Amo 1:11
Oba 13

Tulitarajia na kutarajia kupata msaada kutoka kwa taifa ambalo hali-ngeweza kutuokoa.^a

ⲙ [Tsade]

- 18** Wametuwinda katika kila hatua^b hivi kwamba hatungeweza kutembea kwenye viwanja vya jiji letu.

Mwisho wetu umekaribia; siku zetu zimekwisha, kwa maana mwisho wetu umefika.

ⲙ [Qoph]

- 19** Waliotufuatia walikwenda kasi kuliko tai wa angani.^c

Walitukimbiza milimani; walituvamia nyikani.

ⲙ [Resh]

- 20** Pumzi ya mianzi ya pua zetu, mtiwa-mafuta wa Yehova,^d amenaswa katika shimo lao kubwa,^e Yule tuliyesema hivi kuhusu: “Tutaishi chini ya kivuli chake miongoni mwa mataifa.”

ⲙ [Sin]

- 21** Furahi na kushangilia, Ee binti ya Edomu,^f unayekaa katika nchi ya Usi. Lakini wewe pia utapitishiwa kikombe,^g nawe utalewa na kufunua uchi wako.^h

ⲙ [Taw]

- 22** Adhabu ya dhambi yako, Ee binti ya Sayuni, imekwisha. Hatakupeleka tena uhamishoni.ⁱ Lakini ataukazia uangalifu uovu wako, Ee binti ya Edomu. Atafunua dhambi zako.^j

4:15 *Au “kuishi hapa wakiwa wageni.”

- 5** Kumbuka, Ee Yehova, yale ambayo yametupata. Tazama na uone aibu yetu.^a
- 2** Wageni wamepewa urithi wetu, wageni wamepewa nyumba zetu.^b
- 3** Tumekuwa mayatima, hatuna baba; mama zetu ni kama wajane.^c
- 4** Ni lazima tulipe ili tunywe maji yetu wenyewe,^d na kuni zetu wenyewe tunazinunua.
- 5** Wale wanaotufuatia wamekaribia shingo zetu; Tumechoka, lakini haturuhusiwi kupumzika.^e
- 6** Tunainyooshea mkono Misri^f na Ashuru,^g ili tupate chakula cha kuto-sha.*
- 7** Mababu zetu waliotenda dhambi hawapo tena, lakini ni lazima tuubebe uovu wao.
- 8** Sasa watumishi wanatutawala; hakuna yeyote wa kutunasua kutoka mikononi mwao.
- 9** Tunapata chakula chetu* kwa kuhatarisha uhai wetu,^{#h} kwa sababu ya upanga wa nyikani.
- 10** Ngozi yetu imekuwa moto kama tanuru, kwa sababu ya makali ya njaa.ⁱ
- 11** Wamewafedhehesha* wake walio Sayuni, mabikira walio katika majiji ya Yuda.^j
- 12** Wakuu walitundikwa kwa mikono yao,^k na wazee hawakuheshimiwa.^l

5:6 *Tnn., "mikate ya kutosha ya kula."
5:9 *Tnn., "mikate yetu." #Au "nafsi zetu." 5:11 *Au "Wamewabaka."

SURA YA 5

- a Zb 79:4
Omb 2:15
- b Kum 28:30
Zb 79:1
Yer 6:12
Sef 1:13
- c Kut 22:24
Yer 18:21
- d Kum 28:15, 48
Isa 3:1
Eze 4:11, 16
- e Kum 28:65
- f Isa 30:2
Yer 44:12
Eze 17:17, 18
- g 2Nya 28:16
Yer 2:18, 36
- h Eze 4:10
- i 2Fa 25:3
Omb 4:8
- j Kum 28:30
- k Yer 39:6
- l Isa 47:6
Yer 6:11
Omb 4:16
- Safu ya 2
- a Yos 20:4
- b Yer 25:10
- c Amo 8:10
- d Omb 1:22
- e Kum 28:65
- f Yer 26:18
- g Zb 102:12
Zb 145:13
Zb 146:10
- h Zb 79:5
Yer 14:19
- i Kum 4:30
Zb 80:3
Zb 85:4
Yer 31:18
- j Yer 33:13
- k Kum 28:15

- 13** Vijana wa kiume wanabe-ba jiwe la kusagia, na wawulana wanajikwaa kwa sababu ya kubeba mizigo ya kuni.
- 14** Wazee wametoweka kwenye lango la jiji;^a vijana wa kiume hawapigi muziki wao.^b
- 15** Shangwe imetoweka miyoni mwetu; dansi zetu zimegeuka kuwa maombolezo.^c
- 16** Taji limeanguka kutoka kwenye kichwa chetu. Ole wetu, kwa sababu tumetenda dhambi!
- 17** Kwa sababu hivyo moyo wetu ni mgonjwa,^d Na kwa sababu ya mambo haya macho yetu yamefifia,^e
- 18** Kwa sababu ya Mlima Sayuni, ambao umeachwa ukiwa;^f sasa mbweha wanatangata juu yake.
- 19** Lakini wewe, Ee Yehova, umeketi kwenye kiti chako cha ufalme milele. Kiti chako kinadumu kizazi baada ya kizazi.^g
- 20** Kwa nini unatusahau milele na kutuacha kwa muda mrefu sana hivyo?^h
- 21** Turudishe kwako, Ee Yehova, nasi tutakurudia bila kusita.ⁱ Zifanye siku zetu ziwe mpya kama siku za zamani.^j
- 22** Hata hivyo, umetukataa kabisa. Unaendelea kutukasirikia vikali sana.^k

EZEKIELI

YALIYOMO

- 1 Ezekieli aona maono ya Mungu akiwa Babiloni (1-3)
Maono ya gari la kimbingu la Yehova (4-28)
Dhoruba, wingu, na moto (4)
Viumbe hai wanne (5-14)
Magurudumu manne (15-21)
Anga linalometameta kama barafu (22-24)
Kiti cha ufalme cha Yehova (25-28)
- 2 Ezekieli apewa kazi ya kuwa nabii (1-10)
'Iwe watasikiliza au hawatasikiliza' (5)
Aonyesha kitabu cha kukunjwa chenye nyimbo za huzuni (9, 10)
- 3 Ezekieli aambiwa ale kitabu cha kukunjwa alichopewa na Mungu (1-15)
Ezekieli atakuwa mlinzi (16-27)
Kupuza kunasababisha hatia ya damu (18-21)
- 4 Aonyesha jinsi Yerusalemu litakavyozingirwa (1-17)
Abeba hatia kwa siku 390 na siku 40 (4-7)
- 5 Aonyesha jinsi Yerusalemu litakavyoanguka (1-17)
Nywele za nabii zilizonyolewa zagawanywa katika mafungu matatu (1-4)
Yerusalemu lina uovu kuliko mataifa (7-9)
Waasi waadhibiwa kwa njia tatu (12)
- 6 Dhidi ya milima ya Israeli (1-14)
Sanamu zinazochukiza zitafedheheshwa (4-6)
"Mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova" (7)
- 7 Mwisho umefika (1-27)
Msiba wa pekee (5)
Pesa zatupwa barabarani (19)
Hekalu litatiwa unajisi (22)
- 8 Ezekieli apelekwa Yerusalemu katika maono (1-4)
Vitu vinavyochukiza vyaonekana hekaluni (5-18)
Wanawake wakimlilia Tamuzi (14)
Wanaume wakiabudu jua (16)
- 9 Wanaume sita wanaoangamiza na mwanamume mwenye kidau cha wino (1-11)
Hukumu itaanzia patakatifu (6)
- 10 Moto wachukuliwa kutoka kati ya magurudumu (1-8)
Ufafanuzi kuhusu makerubi na magurudumu (9-17)
Utukufu wa Mungu waondoka hekaluni (18-22)
- 11 Wakuu waovu washutumiwa (1-13)
Jiji lafananishwa na chungu cha kupikia (3-12)
Ahadi ya kurudishwa (14-21)
Wapewa "roho mpya" (19)
Utukufu wa Yehova waondoka Yerusalemu (22, 23)
Ezekieli arudi Ukaldayo katika maono (24, 25)
- 12 Atabiri uhamisho kwa mifano (1-20)
Mizigo ya kwenda uhamishoni (1-7)
Mkuu ataondoka kukiwa na giza (8-16)
Mkate wa wasiwasi, maji ya hofu (17-20)
Msemo wa udanganyifu wathibitika kuwa uwongo (21-28)
"Hakuna neno langu lolote litakalokawia" (28)
- 13 Dhidi ya manabii wa uwongo (1-16)
Kuta zilizopakwa chokaa zitaanguka (10-12)
Dhidi ya manabii wa kike wa uwongo (17-23)
- 14 Wanaoabudu sanamu washutumiwa (1-11)
Hukumu dhidi ya Yerusalemu haiwezi kuepukika (12-23)
Noa, Danieli, na Ayubu waliokuwa waadilifu (14, 20)
- 15 Yerusalemu, mzabibu usiofaa (1-8)
- 16 Upendo wa Mungu kwa Yerusalemu (1-63)
Apatikana kama mtoto aliyeachwa (1-7)
Mungu ampamba na kufanya agano la ndoa pamoja naye (8-14)

- Akosa kuwa mwaminifu (15-34)
Aadhibiwa kama mwanamke mzinzi (35-43)
Alinganishwa na Samaria na Sodoma (44-58)
Mungu akumbuka agano lake (59-63)
- 17 Kitendawili cha tai wawili na mzabibu (1-21)
Chipukizi changa litakuwa mwerezi mkubwa (22-24)
- 18 Kila mtu anawajibika kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe (1-32)
Nafsi inayotenda dhambi itakufa (4)
Mwana hatalipia dhambi ya baba yake (19, 20)
Sifurahishwi na kifo cha mtu mwovu (23)
Toba huhifadhi uhai (27, 28)
- 19 Wimbo wa huzuni kwa ajili ya wakuu wa Israeli (1-14)
- 20 Historia ya uasi wa Waisraeli (1-32)
Ahadi ya kurudishwa kwa Waisraeli (33-44)
Unabii dhidi ya kusini (45-49)
- 21 Upanga wa hukumu wa Mungu wachomolewa (1-17)
Mfalme wa Babiloni kushambulia Yerusalemu (18-24)
Mkuu mwovu wa Israeli ataondolewa (25-27)
"Ulivue taji" (26)
"Mpaka yule aliye na haki ya kisheria atakapokuja" (27)
Upanga utawashambulia Waamoni (28-32)
- 22 Yerusalemu, jiji lenye hatia ya damu (1-16)
Waisraeli ni kama takataka isiyo na thamani (17-22)
Viongozi na watu wa Israeli washutumiwa (23-31)
- 23 Dada wawili ambao si waaminifu (1-49)
Ohola na Ashuru (5-10)
Oholiba na Babiloni na Misri (11-35)
Kuadhibiwa kwa dada wawili (36-49)
- 24 Yerusalemu kama chungu cha kupikia chenye kutu (1-14)
Kifo cha mke wa Ezekiel ni ishara (15-27)
- 25 Unabii dhidi ya Amoni (1-7)
Unabii dhidi ya Moabu (8-11)
- Unabii dhidi ya Edomu (12-14)
Unabii dhidi ya Ufilisti (15-17)
- 26 Unabii dhidi ya Tiro (1-21)
"Uwanja wa kukaushia nyavu za kukokotwa" (5, 14)
Mawe na udongo vyatupwa ndani ya maji (12)
- 27 Wimbo wa huzuni kuhusu meli inayozama ya Tiro (1-36)
- 28 Unabii dhidi ya mfalme wa Tiro (1-10)
"Mimi ni mungu" (2, 9)
Wimbo wa huzuni kuhusu mfalme wa Tiro (11-19)
"Ulikuwa katika Edeni" (13)
"Kerubi anayefunika aliyetiwa mafuta" (14)
'Uovu ulipatikana ndani yako' (15)
Unabii dhidi ya Sidoni (20-24)
Israeli watarudishwa (25, 26)
- 29 Unabii dhidi ya Farao (1-16)
Jiji la Babiloni litapewa Misri kama malipo (17-21)
- 30 Unabii dhidi ya Misri (1-19)
Shambulizi la Nebukadnezar latabiriwa (10)
Nguvu za Farao zavunjwa (20-26)
- 31 Kuanguka kwa Misri, mwerezi mrefu (1-18)
- 32 Wimbo wa huzuni kuhusu Farao na Misri (1-16)
Misri kuzikwa pamoja na wasiotahiriwa (17-32)
- 33 Majukumu ya mlinzi (1-20)
Habari kuhusu kuanguka kwa Yerusalemu (21, 22)
Ujumbe kwa wakaaji wa magofu (23-29)
Watu wapuuzwa ujumbe (30-33)
Ezekiel "kama wimbo wa mapenzi" (32)
"Nabii alikuwa miongoni mwa" (33)
- 34 Unabii dhidi ya wachungaji wa Israeli (1-10)
Jinsi Yehova anavyowatunza kondoo wake (11-31)
"Mtumishi wangu Daudi" atawachunga (23)
"Agano la amani" (25)
- 35 Unabii dhidi ya milima ya Seiri (1-15)
- 36 Unabii kuhusu milima ya Israeli (1-15)

- Kurudishwa kwa Waisraeli (16-38)
 "Nitalitakasa jina langu kuu" (23)
 "Kama bustani ya Edeni" (35)
- 37 Maono ya bonde la mifupa mikavu (1-14)
 Vijiti viwili vitaunganishwa
 pamoja (15-28)
 Taifa moja chini ya mfalme
 mmoja (22)
 Agano la kudumu la amani (26)
- 38 Gogu kushambulia Israeli (1-16)
 Hasira ya Yehova dhidi ya Gogu (17-23)
 'Mataifa yatalazimika kujua kwamba
 mimi ni Yehova' (23)
- 39 Kuangamizwa kwa Gogu na vikosi
 vyake (1-10)
 Mazishi katika Bonde la
 Hamoni-Gogu (11-20)
 Kurudishwa kwa Waisraeli (21-29)
 Roho ya Mungu yamiminiwa juu ya
 Waisraeli (29)
- 40 Ezekieli aletwa Israeli katika
 maono (1, 2)
 Ezekieli aona hekalu kwenye
 maono (3, 4)
 Nyua na malango (5-47)
 Lango la nje la mashariki (6-16)
 Ua wa nje; malango mengine (17-26)
 Ua wa ndani na malango (27-37)
 Vyumba vya utumishi wa
 hekaluni (38-46)
 Madhabahu (47)
 Ukumbi wa hekalu (48, 49)
- 41 Patakatifu pa hekalu (1-4)
 Ukuta na vyumba vya kando (5-11)
 Jengo la magharibi (12)
- Majengo yapimwa (13-15a)
 Sehemu ya ndani ya patakatifu (15b-26)
- 42 Majengo ya vyumba vya kulia
 chakula (1-14)
 Pande nne za hekalu zapimwa (15-20)
- 43 Utukufu wa Yehova wajaa hekaluni (1-12)
 Madhabahu (13-27)
- 44 Lango la mashariki kubaki likiwa
 limefungwa (1-3)
 Maagizo kuhusu wageni (4-9)
 Maagizo kwa ajili ya Walawi na
 makuhani (10-31)
- 45 Mchango mtakatifu na jiji (1-6)
 Sehemu ya kiongozi (7, 8)
 Viongozi watatenda kwa unyooфу (9-12)
 Michango ya watu na ya kiongozi (13-25)
- 46 Matoleo ya pindi mbalimbali (1-15)
 Kurithi mali ya kiongozi (16-18)
 Sehemu za kuchemshia dhabihu (19-24)
- 47 Kijito kinachotiririka kutoka
 hekaluni (1-12)
 Kina cha maji chaongezeka hatua
 kwa hatua (2-5)
 Maji ya Bahari ya Chumvi
 yaponywa (8-10)
 Sehemu zenye majimaji
 haziponywi (11)
 Miti kwa ajili ya chakula na
 kuponya (12)
 Mipaka ya nchi (13-23)
- 48 Kuigawa nchi (1-29)
 Malango 12 ya jiji (30-35)
 Jiji linaloitwa "Yehova Yupo
 Hapo" (35)

1 Katika mwaka wa 30, siku ya tano ya mwezi wa nne, nilipokuwa kando ya mto Kebari^a miongoni mwa watu walihamishwa,^b mbingu zilifunguliwa nami nikaanza kuona maono ya Mungu. **2** Katika siku ya tano ya mwezi huo -yaani, katika mwaka wa tano wa uhamisho wa mfalme Yehoyakini^c— **3** neno la Yehova lilimjia Ezekieli* mwana wa

1:3 *Maana yake "Mungu Huimarisha."

SURA YA 1

a Eze 3:15

b 2Fa 24:12, 14

c 2Nya 36:9, 10

Safu ya 2

a Yer 22:25

b Eze 3:14

c 1Fa 19:11

d Kut 19:18
 Zb 97:2, 3

Buzi kuhani akiwa kando ya mto Kebari katika nchi ya Wakedayo.^a Na huko, mkono wa Yehova ukaja juu yake.^b

4 Nilipokuwa nikitazama, nikaona tufani ya upepo^c iki-ja kutoka kaskazini, na kulikuwa na wingu kubwa na moto unaowakawaka^{*d} uliozungukwa na nuru nyangavu, na katikati ya ule moto kuliku-

1:4 *Au "na radi."

wa na kitu kilichong'aa kama mchanganyiko wa dhahabu na fedha.^a **5** Katikati yake kulikuwa na mfano wa viumbe hai wanne,^b na kila mmoja wao alifanana na mwanadamu. **6** Kila mmoja wao alikuwa na nyuso nne na mabawa manne.^c **7** Miguu yao ilikuwa imenyooka, na nyayo za miguu yao zilikuwa kama nyayo za ndama, nayo ilikuwa ikiing'aa kama shaba iliyong'arishwa.^d **8** Walikuwa na mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao pande zote nne, na wote wanne walikuwa na nyuso na mabawa. **9** Mabawa yao yaligusana. Hawakugeuka walipokuwa wakienda; kila mmoja wao alikuwa akienda mbele moja kwa moja.^e

10 Nyuso zao zilionekana hivi: Kila mmoja wa viumbe hao wanne alikuwa na uso wa mwanadamu na uso wa simba^f upande wa kulia, na uso wa ng'ombe dume^g upande wa kushoto, na kila mmoja wa viumbe hao wanne alikuwa na uso^h wa tai.ⁱ **11** Hivyo ndivyo nyuso zao zilivyokuwa. Mabawa yao yalikuwa yameyoosha juu yao. Kila mmoja wao alikuwa na mabawa mawili yaliyogusana na mabawa mawili yaliyofunika miili yao.^j

12 Kila mmoja wao alikuwa akienda mbele moja kwa moja, walienda popote ambapo roho iliwaelekeza kwenenda.^k Hawakugeuka walipokuwa wakienda. **13** Na wale viumbe hai walionekana kama makaa ya moto yanayowaka, na kitu kilichofanana na mienge ya moto mwangavu kilikuwa kikisonga mbele na nyuma katikati ya hao viumbe hai, na radi ilikuwa ikiwakawaka ku-

SURA YA 1

a Eze 8:2

b Eze 10:9, 15
Ufu 4:6c Isa 6:2
Eze 10:20, 21
Ufu 4:8

d Da 10:5, 6

e Eze 10:11, 15

f 2Sa 17:10
Met 28:1

g Met 14:4

h Eze 10:14, 15
Ufu 4:7

i Ayu 39:27, 29

j Isa 6:2

k Zb 103:20
Ebr 1:7, 14

Safu ya 2

a Da 7:9, 10

b Eze 10:9-13
Ufu 4:7c Met 15:3
Zek 4:10

d Eze 10:15-17

toka katika ule moto.^a **14** Na hao viumbe hai walipoenda na kurudi, mwendo wao ulionekana kama radi inayowakawaka.

15 Nilipoendelea kuwatazama hao viumbe hai, niliona gurudumu moja duniani kando ya kila mmoja wa hao viumbe hai wenye nyuso nne.^b **16** Magurudumu hayo na muundo wake yalionekana yaking'aa kama krisolito, na yote manne yalifanana. Na mwonekano wake na muundo wake ni kama gurudumu lililokuwa ndani ya gurudumu.* **17** Yaliposonga, yangeweza kwenda upande wowote kati ya zile pande nne bila kugeuka walipokuwa yakienda. **18** Mizingo yake ilikuwa juu sana hivi kwamba iliogopesha, na mizingo ya magurudumu yote manne ilikuwa imejaa macho kuizunguka.^c **19** Wakati wowote viumbe hai waliposonga, yale magurudumu yalisonga pamoja nao, na wale viumbe hai walipoinuliwa kutoka duniani, yale magurudumu yaliinuliwa juu pia.^d **20** Walienda popote ambapo roho iliwaelekeza kwenda, popote roho ilipoenda. Magurudumu yaliinuliwa pamoja nao, kwa maana roho iliyokuwa ikitenda katika wale viumbe hai.* ilikuwa pia katika yale magurudumu. **21** Waliposonga, magurudumu hayo yalisonga; na waliposimama tuli, nayo yalisimama tuli; na walipoinuliwa juu kutoka duniani, magurudumu yaliinuliwa juu pamoja nao, kwa maana roho iliyokuwa ikitenda katika wale

1:16 *Labda yalikutana katikati kwenye mhimili mmoja katika pembe mraba.
1:20 *Tnn., "roho ya yule kiumbe hai."

viumbe hai ilikuwa pia katika yale magurudumu.

22 Juu ya vichwa vya wale viumbe hai kulikuwa na mfano wa anga lililometameta kama barafu inayotisha, lililotanda juu ya vichwa vyao.^a

23 Chini ya anga hilo mabawa yao yalikuwa yamenyooka,* moja kuelekea lingine. Kila mmoja alikuwa na mabawa mawili ya kufunika upande mmoja wa mwili wake na mawili ya kufunika upande mwingine. **24** Niliposikia sauti ya mabawa yao, ilikuwa kama sauti ya maji yenye kishindo, kama sauti ya Mweza-Yote.^b Waliposonga, ilikuwa kama sauti ya jeshi. Waliposimama tuli, waliyashusha mabawa yao.

25 Kulikuwa na sauti juu ya anga lililokuwa juu ya vichwa vyao. (Waliposimama tuli, waliyashusha mabawa yao.) **26** Juu ya anga lililokuwa juu ya vichwa vyao kulikuwa na kitu kilichoonekana kama jiwe la yakuti,^c na kilifanana na kiti cha ufalme.^d Kwenye kiti hicho cha ufalme aliketi mmoja aliyeonekana kama mwanadamu.^e **27** Nami nikaona kitu kinachong'aa kama mchanganyiko wa dhahabu na fedha,^f kilichokuwa kama moto unaoing'aa kutoka kwenye kile kilichoonekana kuwa kiuno chake kwenda juu; na kutoka kwenye kiuno chake kwenda chini, nikaona kitu kilichofanana na moto.^g Kulikuwa na mwangaza mkali kumzunguka pande zote **28** kama wa upinde wa mvua^h katika mawingu

1:23 *Au labda, "yalinyooka moja kwa moja."

SURA YA 1

a Eze 10:1

b Zb 29:3
Eze 43:2
Ufu 14:2c Kut 24:10
Zb 96:6
Eze 10:1d 1Fa 22:19
Zb 99:1
Isa 6:1
Ufu 4:2

e Da 7:9

f Eze 8:2

g Kum 4:24
Zb 104:1, 2

h Ufu 4:3

Safu ya 2

a Kut 24:16, 17
Eze 8:4

SURA YA 2

b Da 10:11

c Eze 3:24

d 2Nya 36:15
Eze 33:7e Isa 1:4
Yer 16:12f Kum 9:24
Zb 78:8
Yer 3:25
Mdo 7:51

g Eze 3:7

h Eze 12:2

i Eze 3:11
Eze 33:4, 15
Eze 33:33
Yoh 15:22
Mdo 20:26j 2Fa 1:15
Lu 12:4

k Mik 7:4

l Isa 51:7

m Yer 1:8
Eze 3:9

siku ya mvua. Hivyo ndivyo mwangaza uliozunguka pande zote ulivyoonekana. Ulikuwa kama mwonekano wa utukufu wa Yehova.^a Nilipouona, nikaunguka chini kifudufudi na kuanza kusikia sauti ya mtu akizungumza.

2 Kisha akaniambia: "Mwana wa binadamu,* simama kwa miguu yako ili nizungumze nawe."^b **2** Alipozungumza nami, roho ikaingia ndani yangu na kunifanya nisimame kwa miguu yangu^c ili niweze kumsikia Yule anayezungumza nami.

3 Naye akaendelea kuniambia: "Mwana wa binadamu, ninakutuma kwa watu wa Israeli,^d kwa mataifa yenye kuasi ambayo yameniasi.^e Wao na mababu zao wamenikosea mpaka leo hii.^f **4** Ninakutuma kwa wana wakaidi* na wenyewe moyo mgumu,^g nawe lazima uwaambie, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anavyosema.' **5** Nao, iwe watasikiliza au watakataa kusikiliza—kwa maana wao ni nyumba ya uasi^h—watajua kwa hakika kwamba nabii alikuwa miongoni mwao.ⁱ

6 "Lakini wewe, mwana wa binadamu, usiwaogope,^j na usiogope maneno yao, ingawa umezungukwa na michongoma na miiba*^k na unakaa katikati ya nge. Usiogope maneno yao^l na usitishwe na nyuso zao,^m kwa maana wao ni nyumba ya uasi. **7** Ni lazima

2:1 *"Mwana wa binadamu"; maneno haya yanapatikana mara 93 katika Ezekieli na hapa ndipo yanapopatikana kwa mara ya kwanza. 2:4 *Au "wenye uso mgumu." 2:6 *Au labda, "ingawa watu ni wakaidi, nao ni kama vitu vinavyokudunga."

uwaambie maneno yangu, iwe watasikiliza au la, kwa maana wao ni waasi.^a

8 “Lakini wewe, mwana wa binadamu, sikiliza ninalokuambia. Usiwe mwasi kama nyumba hii ya uasi. Fungua kinywa chako ule ninachokupa.”^b

9 Nilipotazama, niliona mkono ulionyoshwa kunielekea,^c na katika mkono huo niliona kitabu cha kukunjwa kilichoandikwa.^d **10** Alipokikunjwa mbele yangu, kilikuwa kimeandikwa mbele na nyuma.^e Nyimbo za huzuni na maombolezo na vilio vilikuwa vimeandikwa kwenye kitabu hicho.^f

3 Kisha akaniambia: “Mwana wa binadamu, kula kilicho mbele yako.* Kula kitabu hiki cha kukunjwa, na uende ukazungumze na watu wa nyumba ya Israeli.”^g

2 Kwa hiyo nikafungua kinywa changu, naye akani pa kitabu hicho nile. **3** Naye akaendelea kuniambia: “Mwana wa binadamu, kula kitabu hiki ninachokupa, ukijaze tumboni mwako.” Basi nikaaanza kukila, nacho kilikuwa kitamu kama asali kinywani mwangu.^h

4 Akaniambia: “Mwana wa binadamu, nenda miongoni mwa watu wa nyumba ya Israeli uwaambie maneno yangu. **5** Kwa maana hutumwi kwenda kwa watu wanaozungumza lugha isiyoeleweka au lugha isiyojulikana, bali kwa watu wa nyumba ya Israeli. **6** Hutumwi kwa watu wengi wanaozungumza lugha isiyoeleweka au lugha isiyojulikana

SURA YA 2

a Yer 1:17

b Yer 15:16
Ufu 10:9, 10

c Yer 1:9

d Eze 3:1

e Ufu 5:1

f Eze 19:1

SURA YA 3

g Ufu 10:9, 10

h Zb 119:103
Yer 15:16
Ufu 10:9, 10

Safu ya 2

a Yon 3:4, 5
Mt 11:21

b Lu 10:16

c Kut 34:9
Yer 3:3
Yer 5:3

d Yer 1:18, 19
Yer 15:20
Mik 3:8

e Isa 50:7

f Yer 17:18

g 2Fa 24:12, 14

h Eze 2:5

i Eze 8:3

j Eze 1:24

k Eze 10:16

na, ambao maneno yao huwezi kuelewa. Ikiwa ningekutumama kwao, wangekusikiliza.^a

7 Lakini watu wa nyumba ya Israeli watakataa kukusikiliza, kwa maana hawataki kunisikiliza mimi.^b Watu wote wa nyumba ya Israeli wana vichwa vigumu na mioyo migumu.^c **8** Tazama! Nimeufanya uso wako uwe mgumu kama nyuso zao na paji la uso wako liwe gumu kama mapaji ya nyuso zao.^d **9** Nimeelifanya paji la uso wako kuwa kama almasi, gumu kuliko jiwe gumu.^e Usiwaogope, wala usitishwe na nyuso zao,^f kwa maana wao ni nyumba ya uasi.”

10 Naye akaendelea kuniambia: “Mwana wa binadamu, yatie moyoni mwako na kuyasikiliza maneno yangu yote nitakayokuambia. **11** Nenda miongoni mwa watu wako waliohamishwa*^g uzungumze nao. Waambie, ‘Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anavyosema,’ iwe watasikiliza au watakataa kusikiliza.”^h

12 Ndipo roho ikanibebaⁱ nami nikasikia nyuma yangu sauti ya mngurumo mkubwa iliyosema: “Utukufu wa Yehova na usifiwe katika mahali pake.” **13** Nilisikia sauti ya mabawa ya wale viumbe hai yalipokuwa yakigusana,^j na sauti ya magurudumu kando yao,^k na sauti ya mngurumo mkubwa. **14** Nayo roho ikanibeba na kunicukua, nami nikaenda kwa uchungu na kwa ghadhabu ya roho yangu, na mkono wa Yehova ukatulia juu yangu kwa nguvu.

3:1 *Tnn., “kula utakachopata.”

3:11 *Tnn., “wana wa watu wako.”

15 Basi nikaenda Tel-abibu kwa watu waliohamishwa, waliokuwa wakikaa kando ya mto Kebari,^a nami nikakaa huko walipokuwa wakikaa; nika-kaa miongoni mwao kwa siku saba nikiwa nimepigwa na bum-buazi.^b

16 Mwishoni mwa siku saba neno la Yehova likanijia:

17 “Mwana wa binadamu, nimekuweka kuwa mlinzi wa watu wa nyumba ya Israeli;^c nawe unaposikia neno kutoka katika kinywa changu, lazima uwape onyo langu.^d **18** Nina-pomwambia mtu mwovu, ‘Hakika utakufa,’ lakini wewe usimwonye, nawe ukatae ku-mwambia mtu huyo mwovu aiache njia yake ya uovu ili aendelee kuwa hai,^e yeye atakufa kwa sababu ya kosa lake kwa sababu yeye ni mwovu,^f lakini damu yake nitaidai kutoka kwako.*^g **19** Lakini ukimwonya mtu mwovu naye asiuche uovu wake na njia yake ya uovu, yeye atakufa kwa sababu ya kosa lake, lakini wewe kwa hakika utauokoa uhai wako.*^h

20 Lakini mtu mwadilifu anapochua uadilifu wake na kutenda kosa,[#] nitaweka kikwazo mbele yake, naye atakufa.ⁱ Ikiwa hukumwonya, atakufa kwa sababu ya dhambi yake na matendo yake ya uadilifu hayatakumbukwa, lakini damu yake nitaidai kutoka kwako.*^j **21** Lakini ikiwa umemwonya mtu mwadilifu asitende dhambi, naye asitende dhambi, kwa hakika atae-

3:18, 20 *Au “nitakufanya uwajibike kwa sababu ya damu yake.” 3:19, 21 *Au “utaiokoa nafsi yako.” 3:20 #Au “kutenda jambo lisilo la haki.”

SURA YA 3

a Eze 1:3

b Yer 23:9

c Isa 21:8
Isa 62:6
Yer 6:17d Isa 58:1
Eze 33:7e Mdo 2:40
1Ti 4:16

f Eze 33:4

g Eze 33:8

h Eze 33:9
Mdo 18:6
Mdo 20:26i Eze 18:24, 26
Eze 33:12, 18j Law 19:17
Eze 33:6
Ebr 13:17

Safu ya 2

a Met 17:10
Eze 33:14, 15
Yak 5:19, 20

b Eze 1:27, 28

c Eze 1:1

d Eze 2:2
Da 10:19e Eze 24:27
Eze 33:22

f Mt 11:15

g Isa 30:9

SURA YA 4

h 2Fa 24:11
Yer 39:1

i 2Fa 25:1

j Yer 6:6
Yer 32:24

k Eze 21:22

ndelea kuwa hai kwa sababu alionywa,^a na wewe utauokoa uhai wako.”*

22 Nikiwa huko mkono wa Yehova ukanijia, naye akania-mbia: “Ondoka, nenda kwenye bonde tambarare, nami nitazungumza nawe huko.”

23 Basi nikaondoka na kwenye bonde tambarare, na tazama! utukufu wa Yehova ulikuwa huko,^b kama utukufu niliokuwa nimeuona kando ya mto Kebari,^c nami nikaanguka chini kifudifudi. **24** Kisha roho ikaingia ndani yangu na kunifanya nisimame kwa mi-guu yangu,^d naye akaniambia:

“Nenda, jifungie ndani ya nyumba yako. **25** Lakini wewe mwana wa binadamu, wataweka kamba juu yako na kukufunga nazo ili usiweze kuondoka miongoni mwao.

26 Nami nitaufanya ulimi wako ushikamane na kaakaa la kinywa chako, nawe utakuwa bubu, usiweze kuwakaripia, kwa sababu wao ni nyumba ya uasi. **27** Lakini nina-pozungumza naye nitafungua kinywa chako, nawe lazima uwaambie,^e ‘Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anavyosema.’ Anayesikiliza na asikilize,^f na anayekataa kusikiliza na akatae, kwa sababu wao ni nyumba ya uasi.^g

4 “Na wewe, mwana wa binadamu, chukua tofali na uliweke mbele yako. Uchonge jiji juu yake—Yerusalemu. **2** Lizingire na ujenge ukuta wa kulizingira,^h utengeneze boma la kulizingira,ⁱ upige kambi kulizunguka,^j na kulizungushia mitambo ya kubomolea.^k **3** Chukua kioeko cha chuma, na ukiweke kuwa ukuta wa chuma kati yako na jiji

hilo. Kisha ukaze uso wako dhidi yake, nalo litazingirwa; nawe utalizingira. Hiyo ni ishara kwa watu wa nyumba ya Israeli.^a

4 “Kisha ulalie upande wako wa kushoto na uweke hatia ya watu wa nyumba ya Israeli juu yako.^{*b} Utabeba hatia yao kwa idadi ya siku utakazolalia upande wako wa kushoto. **5** Na mimi nitakupa wewe siku 390, zinazolingana na miaka ya hatia yao,^c nawe utaipeba hatia ya watu wa nyumba ya Israeli. **6** Nawe lazima uzitimize.

“Kisha kwa mara ya pili utalala chini, utalalia upande wako wa kulia, nawe utaipeba hatia ya watu wa nyumba ya Yuda^d kwa siku 40. Nimekupa wewe siku moja kwa mwaka mmoja, siku moja kwa mwaka mmoja. **7** Nawe utaelezeke uso wako kwa jiji la Yerusalemu lililozingirwa,^e mkono wako ukiwa wazi, nawe utatabiri dhidi ya jiji hilo.

8 “Tazama! Nitakufunga kwa kamba ili usiweze kugeuka kutoka upande mmoja kwenenda upande mwingine, mpa-ka utakapotimiza siku zako za kulizingira.

9 “Na uchukue ngano, shayiri, maharagwe mapana, den-
gu, mtama, na kusemethi, nawe uvitie katika chombo kimoja na ujitengenezee mkate. Kwa idadi ya siku unazolalia upande wako, siku 390, utaula.^f **10** Utapima na kula shekeli 20* za chakula kwa siku. Utaula nyakati hususa.

4:4 *Tnn., “juu yake,” yaani, upande wa kushoto wa Ezekieli. 4:10 *Karibu gramu 230. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 4

a Eze 12:6
Eze 24:24

b 2Fa 17:21

c Hes 14:34
1Fa 12:19, 20

d 2Fa 23:27

e Yer 52:4

f Eze 4:5

Safu ya 2

a Ho 9:3

b Kut 22:31
Law 7:24
Law 11:40

c Kum 14:3
Isa 65:4
Isa 66:17

d Law 26:26
Isa 3:1
Eze 5:16

e 2Fa 25:3
Yer 37:21
Omb 1:11
Omb 4:9
Omb 5:9, 10

f Eze 12:18

11 “Na utakunywa maji kwa kipimo, sehemu ya sita ya hini.* Utayanywa nyakati hususa.

12 “Utaula kama ambavyo ungekula mkate wa mviringo wa shayiri; utauoka mbele ya macho yao, ukitumia mavi ya wanadamu yaliyokauka.”

13 Na Yehova akaendelea kusema: “Hivyo ndivyo Waisraeli watakvuola mkate wao—usio safi—kati ya mataifa ambako nitawatawanyana.”^a

14 Ndipo nikasema: “Isiwe hivyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Tangu ujana wangu mpaka sasa sijatiwa* unajisi kwa kula nyama ya mnyama ambaye amepatikana amekufa wala mnyama aliyeruliwa,^b na nyama isiyo safi[#] haijawahi kuingia kinywani mwangu.”^c

15 Basi akaniambia: “Sawa, nitakuruhusu utumie mavi ya ng’ombe badala ya mavi ya wanadamu, nawe utaoka mkate wako juu yake.” **16** Naye akaniambia: “Mwana wa binadamu, nitafanya chakula kikosekane* Yerusalemu,^d na kwa wasiwasi mwingi wataku-
kula mkate wao kwa kipimo,^e na kwa hofu nyingi watakunywa maji yao kwa kipimo.^f **17** Hili litatukia ili wakose mkate na maji, nao waangalia-
ne kwa mshtuko na kudhoofika kwa sababu ya kosa lao.

5 “Lakini wewe, mwana wa binadamu, chukua upanga mkali ili utumie kama wembe wa kinyozi. Nyoa kichwa chako na ndevu zako, nawe

4:11 *Karibu lita 0.6. Angalia Nyongeza B14. 4:14 *Au “nafsi yangu haijatiwa.”
#Au “mbaya.” 4:16 *Tnn., “nitazivunja fito za mikate.” Labda ni fito zilizotumiwa kuhifadhia mikate.

uchukue mizani, uzipime nywele hizo na kuzigawa katika mafungu. **2** Utaiteketeza theluthi moja ya nywele hizo katika moto ndani ya jiji siku za kuzingira zitakapokamili-ka.^a Kisha utachukua theluthi nyingine nawe utaipiga kwa upanga kulizunguka jiji pande zote,^b na theluthi ya mwisho utaitawanya kwenye upepo, nami nitauchomoa upanga ili kuwakimbiza.^c

3 “Pia utachukua nywele chache na kuzifunga katika pindo za* vazi lako. **4** Na uchukue nyingine na kuzitupa motoni na kuziteketeza. Moto utatokea humo na kuenea katika nyumba yote ya Israeli.^d

5 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Huyu ni Yerusalemu. Nimemweka katikati ya mataifa, na nchi zinamzunguka pande zote. **6** Lakini aliasi sheria zangu* na amri zangu, akatenda uovu zaidi kuliko mataifa na nchi zinazomzunguka pande zote.^e Kwa maana wamekataa sheria zangu, nao hawakutembea katika amri zangu.’

7 “Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu mlikuwa wambufu kuliko mataifa yote yanayowazunguka na hamkutembea katika amri zangu au kutenda kulingana na sheria zangu, badala yake mkafuata sheria za mataifa yanayowazunguka pande zote.^f **8** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Sasa niko dhidi yako, Ee jiji,^g na mimi mwenyewe nitatekeleza hukumu katikati yako mbele ya mataifa.^h

5:3 *Au “marinda ya.” 5:6 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

SURA YA 5

a Yer 9:21
Eze 4:8

b Yer 15:2

c Law 26:33
Eze 5:12

d Yer 4:4

e Eze 16:46, 47

f 2Fa 21:9, 11
Yer 2:11

g Yer 21:5
Eze 15:7

h Kum 29:22, 24
1Fa 9:8
Omb 2:15

Safu ya 2

a Omb 4:6
Da 9:12

b Law 26:29
Yer 19:9
Omb 4:10

c Law 26:33
Kum 28:64

d Law 20:3
2Fa 21:1, 7
2Nya 36:14
Yer 32:34

e Omb 2:21
Eze 7:4

f Yer 14:12
Yer 15:2
Yer 21:9

g Law 26:33
Yer 9:16
Yer 42:16

h Eze 16:42

i Kut 20:3, 5
Kut 34:14
Kum 6:15

j Kum 28:37
1Fa 9:7
Ne 2:17

k Zb 79:4
Yer 24:9
Omb 2:15
Omb 3:61, 62

9 Nami nitafanya ndani yako mambo ambayo sijawahi kufanya, na ambayo sitafanya tena kwa sababu ya mazoea yako yote yanayochukiza.^a

10 ““Kwa hiyo akina baba miongoni mwenye watawala wana wao,^b nao wana watawala baba zao, nami nitatekeleza hukumu kati yenu na kuwatawanya kila upande* wale waliobaki kati yenu.”^c

11 ““Kwa hiyo, kwa hakika, kama ninavyoishi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘kwa sababu mlipachafua mahali pangu patakatifu kwa sanamu zenu zote zinazochukiza na mazoea yenu yote yanayochukiza,^d mimi pia nitawakataa;* jicho langu halitasikitika, nami sitawahurumia.^e **12** Theluthi yenu moja watakufa kwa ugonjwa hatairi au kuangamia kwa njaa kali miongoni mwenu. Na theluthi nyingine watauawa kwa upanga kuwazunguka pande zote.^f Nami nitaitawanya theluthi ya mwisho kila upande,* nami nitauchomoa upanga ili kuwakimbiza.^g **13** Ndipo hasira yangu itakapokoma, na ghadhabu yangu dhidi yao itatulia, nami nitaridhika.^h Nitakapomaliza kuwamwagia ghadhabu yangu, watalazimika kujua kwamba mimi, Yehova, ninasisitiza watu waniabudu mimi peke yangu.ⁱ

14 ““Nitakufanya kuwa ukiwa na kitu cha kushutumiwa kati ya mataifa yanayokuzunguka na mbele ya macho ya kila mpita njia.^j **15** Utakuwa kitu cha kushutumiwa na kudharauliwa,^k mfano wa kuo-

14 ““Nitakufanya kuwa ukiwa na kitu cha kushutumiwa kati ya mataifa yanayokuzunguka na mbele ya macho ya kila mpita njia.^j **15** Utakuwa kitu cha kushutumiwa na kudharauliwa,^k mfano wa kuo-

5:10, 12 *Tnn., “kuelekea kila upepo.” 5:11 *Au “nitawapunguza.”

nya na tisho kwa mataifa yanayokuzunguka, nitakapotekeleza hukumu dhidi yako kwa hasira na ghadhabu na kwa adhabu kali. Mimi, Yehova, nimesema.

16 “Nitawaletea mishale hatari ya njaa kali ili iwaangamize.^a Mishale nitakayowaletea itawaangamiza ninyi. Nitaifanya njaa iwe kali zaidi kwenu kwa kufanya chakula chenu kisipatikane.*^b **17** Nitawaletea njaa kali na wanyama wakali wa mwituni,^c nao watawaua watoto wenu. Ugonjwa hatari na umwagaji wa damu utawalemea, nami nitaleta upanga dhidi yenu.^d Mimi, Yehova, nimesema.”

6 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako kwenye milima ya Israeli na utabiri dhidi yake. **3** Nawe utasema, ‘enyi milima ya Israeli, sikieni neno la Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova: Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anavyoiambia milima, vilima, vilito na mabonde: “Tazameni! Ninaleta upanga dhidi yenu, nami nitaharibu mahali penu pa juu. **4** Madhabahu zenu zitabomolewa na vinara vyenu vya uvumba vitavunjwa,^e na waliouawa kati yenu nitawatupa chini mbele ya sanamu zenu zinazochukiza.*^f **5** Nami nitazitupa maiti za watu wa Israeli mbele ya sanamu zao zinazochukiza, nami nitaitawanya mifupa yenu kuzunguka pande zote za madhabahu

5:16 *Tnn., “kwa kuvunja fito zenu za mikate.” Labda ni fito zilizotumiwa kuhifadhia mikate. 6:4 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

SURA YA 5

a Kum 32:23

b Law 26:26
Eze 4:16c Law 26:22
Kum 32:24
Eze 14:21
Eze 33:27

d Eze 21:3

SURA YA 6

e Isa 27:9

f Law 26:30

Safu ya 2

a Yer 8:1, 2

b Yer 2:15
Yer 32:29
Mik 3:12

c Eze 16:39

d Yer 14:18

e Eze 7:4

f Yer 30:10
Yer 44:28
Eze 14:22g Kum 30:1, 2
Zb 137:1h Zb 78:40, 41
Isa 63:10

i Hes 15:39

j Eze 20:43
Eze 36:31k Eze 33:29
Da 9:12
Zek 1:6l Yer 15:2
Yer 16:4
Eze 5:12

zenu.^a **6** Katika makao yenu yote, majiji yataharibiwa^b na mahali pa juu patabomolewa na kuachwa ukiwa.^c Madhabahu zenu zitaharibiwa na kuvunjwa vipandevipande, sanamu zenu zinazochukiza zitaharibiwa, vinara vye-nu vya uvumba vitakatwakatwa, na kazi zenu zitafutiliwa mbali. **7** Na wale waliouawa wataunguka katikati yenu,^d nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^e

8 ““Lakini nitaacha wengine wabaki, kwa maana baadhi yenu wataponyoka upanga miongoni mwa mataifa mtakapotawanywa katika nchi mbalimbali.^f **9** Na wale wataoonyoka watanikumbuka kati ya mataifa ambamo watapelekwa mateka.^g Wataambua kwamba nilikuwa nimevunjika moyo kwa sababu ya moyo wao usio na uamini-fu* ulioniacha^h na macho yao ambayo yanatamani sana[#] sanamu zao zinazochukiza.ⁱ Wataaibika na kuchukizwa na mambo yote maovu na yenye kuchukiza ambayo wameten-^jnda.^j **10** Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova na kwamba vitisho vyangu vya kuwaletea msiba huu havikuwa vya bure.”^k

11 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Piga makofi na upige mguu chini, na uomboleze kwa sababu ya mambo yote maovu na yanayochukiza yaliyofanywa na watu wa nyumba ya Israeli, kwa maana watakufa kwa upanga, kwa njaa kali na kwa ugonjwa hatari.^l **12** Yule

6:9 *Au “ulipotoka kimaadili; wa uka-haba.” #Au “yanayofuatilia kwa upotovu wa kimaadili.”

aliye mbali sana atakufa kwa ugonjwa hatari, na yule aliye karibu atauawa kwa upanga, na yeyote anayeponyoka mambo hayo na kubaki atakufa kwa njaa kali; nami nitawawagia kikamili ghadhabu yangu.^a **13** Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova^b wakati waliouawa miongoni mwao watakapotapakaa kati ya sanamu zao zinazochukiza kuzunguka pande zote za madhabahu zao,^c juu ya kila kilima kirefu, juu ya vilele vyote vya milima, na chini ya kila mti wenye majani mengi, na chini ya matawi ya miti mikubwa, mahali ambapo wametoa dhabihu zenye harufu nzuri* ili kuzituliza sanamu zao zote zinazochukiza.^d **14** Nami nitauyoosha mkono wangu dhidi yao na kuifanya nchi iwe ukiwa, na makao yao yote yatakuwa ukiwa kuliko nyika iliyo karibu na Dibla. Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

7 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Nawe Mwana wa binadamu, hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anavyoiambia nchi ya Israeli: ‘Mwisho! Mwisho umezifikia pembe nne za nchi. **3** Sasa mwisho umekufikia, nami nitakumwagia hasira yangu, nami nitakuhukumu kulingana na njia zako na kukua-dhibu* kwa sababu ya matendo yako yote yanayochukiza. **4** Jicho langu halitakusikitikia; wala sitakuhurumia,^e kwa maana nitakuletea matokeo ya njia zako mwenyewe, nawe utapatwa na madhara ya ma-

6:13 *Au “wametoa harufu zinazovutia.”
7:3, 8 *Au “kukufanya uwajibike.”

SURA YA 6

a Eze 5:13

b Eze 12:15

c Yer 8:2

d Eze 20:28

SURA YA 7

e Eze 5:11

Safu ya 2

a Yer 16:18
Eze 16:43

b Eze 6:13

c 2Fa 21:12
Da 9:12

d Sef 1:14

e 2Nya 34:21

f Yer 7:20
Eze 5:13

g Yer 13:14

h Isa 66:6
Eze 33:29

i Sef 1:14

j Isa 59:6
Yer 6:7
Mik 6:12

k Sef 1:18

tendo yako yanayochukiza.^a Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^b

5 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Tazama! Msiba, msiba wa pekee, unakuja.^c **6** Mwisho unakuja; mwisho utakuja; utainuka* wenyewe dhidi yako. Tazama! Unakuja. **7** Zamu yako imefika,* wewe unayekaa nchini. Wakati unakuja, siku hiyo iko karibu.^d Kuna vurugu, wala si kelele za shangwe milimani.

8 “‘Hivi karibuni nitakumwagia ghadhabu yangu,^e nami nitakumwagia hasira yangu yote,^f nami nitakuhukumu kulingana na njia zako na kukua-dhibu* kwa sababu ya matendo yako yote yanayochukiza. **9** Jicho langu halitakusikitikia; wala sitakuhurumia.^g Kwa maana nitakuletea matokeo ya njia zako mwenyewe, nawe utapatwa na madhara ya matendo yako mwenyewe yanayochukiza. Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi, Yehova, ndiye ninayewapiga.^h

10 “‘Tazama, ile siku! Tazama, inakuja!ⁱ Zamu yako imefika;* fimbo imechanua na kimbelebele kimechipuka. **11** Ukatili umesitawi na kuwa fimbo ya uovu.^j Wao wenyewe, mali yao, umati wao, wala umashuhuri wao hautaokoka. **12** Wakati utakuja, siku hiyo itafika. Mnunuzi asishangilie, na muuzaji asiomboleze, kwa maana kuna ghadhabu dhidi ya umati wao wote.*^k **13** Kwa maana muuzaji hata-

7:6 *Tnn., “utaamka.” 7:7, 10 *Au labda, “Shada lako la maua limefika.” 7:12 *Yaani, wale wanaonunua mali na pia wale wanaouza hawatafaidika, kwa maana wote wataangamizwa.

kirudia kitu alichouza, hata uhai wake ukiokolewa, kwa maana maono hayo yanahusu umati wote. Hakuna atakayerudi, na kwa sababu ya kosa lake,* hakuna atakayeoka uhai wake.

14 “Wamepiga tarumbeta^a na kila mtu yuko tayari, lakini hakuna anayeenda vitani, kwa sababu nina ghadhabu dhidi ya umati wote.^b

15 Upanga uko nje,^c na ugonjwa hatari na njaa kali zimo ndani. Yeyote aliye uwanjani atakufa kwa upanga, na njaa kali na ugonjwa hatari vitawameza wale walio jijini.^d

16 Watu wao watakaofanikiwa kuponyoka wataenda milimani, na kama njiwa wa mabondeni, kila mmoja ataomboleza kwa sababu ya kosa lake.^e

17 Mikono yao yote italegea, na magoti yao yote yatadondosha maji.^{*f} **18** Wamevaa nguo za magunia,^g nao wanatetemeka.* Kila mtu ataabishwa, na kila kichwa kitakuwa na upara.^{#h}

19 “Watatupa fedha yao barabarani, nayo dhahabu yao itawachukiza. Wala fedha yao wala dhahabu yao haitaweza kuwaokoa katika siku ya ghadhabu ya Yehova.ⁱ Hawatashiba,* wala kuyajaza matumbo yao, kwa maana vitu hivyo[#] vimekuwa kikwazo kinachosababisha kosa lao. **20** Walijivunia urembo wa mapambo yao, nao waka-

7:13 *Au labda, “kwa kosa lake.” **7:17** *Yaani, watajikojolea kwa sababu ya woga. **7:18** *Tnn., “wamefunikwa na hofu.” #Yaani, vichwa vyao vitanyolewa kwa sababu ya maombolezo. **7:19** *Au “Nafsi zao hazitashiba.” #Yaani, fedha yao na dhahabu yao.

SURA YA 7

a Yer 4:5

b Yer 7:20
Yer 12:12

c Law 26:25

d Yer 14:18
Eze 5:12

e Isa 59:11

f Eze 21:7

g Isa 3:24

h Isa 22:12

i Met 11:4
Sef 1:18

Safu ya 2

a 2Fa 21:1, 7
Yer 7:30

b Yer 18:17

c 2Nya 36:19
Omb 1:10d Yer 39:6, 7
Omb 3:7e 2Fa 21:16
2Fa 24:3, 4
Yer 2:34
Eze 9:9f Isa 59:6
Mik 2:2g Kum 28:48-51
Eze 21:31
Hab 1:6h Yer 6:12
Omb 5:2

i Eze 21:2

j Isa 57:21
Yer 8:15k Yer 21:1, 2
Yer 37:17l Zb 74:9
Omb 2:9
Eze 20:3

m Yer 52:10

yatumia* kutengeneza mifano yao inayochukiza, sanamu zao zinazochukiza.^a Ndiyo sababu nitaifanya fedha na dhahabu yao kuwa chukizo kwao. **21** Nami nitaitia* mikononi mwa wageni ili waipore na kuwapa waovu wa dunia kuwa nyara, nao wataitia unajisi.

22 “Nami nitaugueza uso wangu kutoka kwao,^b nao watapatia unajisi mahali pangu palipofichika,* na wanyang’anyi wataingia mahali hapo na kupatia unajisi.^c

23 “Tengeneza mnyororo,^{*d} kwa maana nchi imejaa hukumu yenye madoa ya damu^e na jiji limejaa ukatili.^f **24** Nami nitaingiza mataifa mabaya kabisa,^g nayo yatamiliki nyumba zao,^h nami nitakikomesha kiburi cha wenye nguvu, na mahali pao patakatifu patatiwa unajisi.ⁱ

25 Maumivu yao yatakapokuja, watatafuta amani lakini haitakuwepo.^j **26** Msiba utakuja juu ya msiba, na habari baada ya habari, na watu watatafuta maono kutoka kwa nabii,^k lakini sheria itatoweka* kutoka kwa kuhani na ushauri[#] kutoka kwa wazee.^l **27** Mfalme ataomboleza,^m naye mkuu atavaa kukata tamaa,* na mikononi ya watu wa nchi itatetemeka kwa hofu. Nitawatendea kulingana na njia zao, nami nitawahukumu kama walivyohukumu.

7:20 *Yaani, mapambo ya dhahabu na fedha. **7:21** *Yaani, fedha yao na dhahabu yao walivyotumia kutengeneza sanamu. **7:22** *Inaonekana ni sehemu ya ndani zaidi ya mahali patakatifu pa Yehova. **7:23** *Yaani, minyororo ya utekwa. **7:26** *Au “mafundisho yatatoweka.” #Au “mashauri.” **7:27** *Au “ukiwa.”

Nao watalazimika kujua kwa mba mimi ni Yehova.”^a

8 Na katika mwaka wa sita, mwezi wa sita, siku ya tano ya mwezi huo, nilipokuwa nimeketi nyumbani mwangu na wazee wa Yuda walipokuwa wameketi mbele yangu, mkono wa Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ulinishika nikiwa hapo. **2** Nilipokuwa nitazama, niliona umbo lili loonekana kama moto; kulikuwa na moto chini ya kitu kilichoonekana kama kiuno chake,^b na kuanzia kiuno chake kwenda juu, mwonekano wake uling'aa kama mchanganyiko wa dhahabu na fedha.^c **3** Kisha akanyoosha kitu kilichoonekana kama mkono na kuniinua kwa kishungi cha nywele za kichwa changu, na roho ikanibeba katikati ya dunia na mbingu na kunileta Yerusalemu kupitia maono kutoka kwa Mungu, kwenye njia inayoelekea kwenye lango la ndani^d linalotazama kaskazini, mahali ilipokuwa ishara ya* ibada ya sanamu inayochochea wivu.^e **4** Na tazama! utukufu wa Mungu wa Israeli ulikuwa hapo,^f kama mwonekano niliokuwa nimeuona katika bonde tambarare.^g

5 Kisha akaniambia: “Mwana wa binadamu, tafadhali inua macho yako kuelekea kaskazini.” Basi nikainua macho yangu kuelekea kaskazini, na huko, upande wa kaskazini wa lango la madhabahu kulikuwa na ishara hii ya* wivu langoni. **6** Naye akaniambia: “Mwana wa binadamu, je, unaona mambo ma-

8:3 *Au “mfano wa.” **8:5** *Au “mfano huu wa.”

SURA YA 7
a Eze 6:13

SURA YA 8
b Da 7:9

c Eze 1:4, 27

d Yer 20:2
Eze 9:2

e Kum 32:16

f Kut 40:34

g Eze 1:27, 28

Safu ya 2
a 2Nya 36:14

b Yer 26:4, 6

c Law 11:10

d Kut 20:4, 5

e 2Fa 22:3, 4
2Fa 25:22
Yer 26:24

f Eze 16:17, 18

baya sana na yenye kuchukiza ambayo watu wa nyumba ya Israeli wanafanya hapa,^a mambo yanayonifanya niende mbali sana na mahali pangu patakatifu?^b Lakini utao-na mambo yanayochukiza ya-liyo mabaya hata zaidi.”

7 Kisha akanileta kwenye mlango wa ua, nami nilipotazama, niliona tundu ukutani. **8** Akaniambia: “Mwana wa binadamu, tafadhali toboa ukuta.” Nami nikautoboa ukuta na kuona mlango. **9** Akaniambia: “Ingia ndani uone mambo maovu na yenye kuchukiza wanayofanya hapa.” **10** Basi nikaingia na kutazama, nikaona mifano mbalimbali ya viumbe wanaotambaa na wanyama wanaochukiza^c na sanamu zote zinazochukiza* za watu wa nyumba ya Israeli;^d zilikuwa zimechongwa ukutani kuzunguka pande zote. **11** Na wazee 70 wa nyumba ya Israeli walikuwa wamesimama mbele ya vitu hivyo, naye Yaazania mwana wa Shafani^e alikuwa amesimama miongoni mwao. Kila mmoja wao alikuwa na chetezo chake mkononi mwake, na wingu la uvumba lenye manukato lilikuwa likipanda juu.^f **12** Akaniambia: “Mwana wa binadamu, je, umeona mambo ambayo wazee wa nyumba ya Israeli wanafanya gizani, kila mmoja akiwa katika vyumba vya ndani ambamo sanamu zake za kuchongwa zimewekwa ili zionekane?* Kwa maana wanasema, ‘Yeho-

8:10 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau. **8:12** *Au “katika vyumba vya ndani vya sanamu yake bora?”

va hatuoni. Yehova ameiacha nchi hii.”^a

13 Naye akaendelea kuniambia: “Utaona mambo yanayochukiza yaliyo mabaya hata zaidi ambayo wanafanya.”

14 Basi akanileta kwenye njia inayoelekea kwenye lango la kaskazini la nyumba ya Yehova, na huko nikaona wanawake wameketi wakimlilia mungu Tamuzi.

15 Naye akaendelea kuniambia: “Je, unaona mambo haya, ewe mwana wa binadamu? Utaona mambo yanayochukiza ambayo ni mabaya hata zaidi kuliko haya.”^b

16 Basi akanileta katika ua wa ndani wa nyumba ya Yehova.^c Hapo kwenye mlango wa hekalu la Yehova, katikati ya ukumbi na madhabahu, kulikuwa na wanaume 25 hivi ambao migongo yao ilielekea hekalu la Yehova na nyuso zao zilitazama mashariki; nao walikuwa wakiliinamia jua kuelekea mashariki.^d

17 Akaniambia: “Mwana wa binadamu, je, unaona hili? Je, ni jambo dogo sana kwa watu wa nyumba ya Yuda kufanya mambo haya yanayochukiza, kuijaza nchi ukatili^e na kuelekea kunikasirisha? Tazama, wanaidunga pua yangu kwa lile tawi.”^f **18** Basi nitenda kwa ghadhabu. Jicho langu halitasikitika; wala sita-wahurumia.^f Hata wakilia kwa sauti kubwa masikioni mwangu, sitawasikia.”^g

9 Kisha nikamsikia akisema hivi kwa sauti kubwa: “Waiteni wale watakaoliadhibu jiji hili, kila mmoja wao aki-

8:17 *Inaonekana ni tawi lililotumiwa katika ibada ya sanamu.

SURA YA 8

a Isa 29:15
Eze 9:9

b 2Nya 36:14

c 2Nya 4:9

d Kum 4:19
2Fa 17:16
Yer 8:1, 2

e 2Fa 21:16
Yer 19:4
Eze 9:9

f Eze 5:11
Eze 7:9

g Isa 1:15
Mik 3:4

Safu ya 2

SURA YA 9

a Yer 20:2
Eze 8:3

b 2Nya 4:1

c Eze 3:23
Eze 8:3, 4
Eze 11:22

d Eze 10:4

e Zb 119:53
2Pe 2:7, 8

f Eze 5:11

g Kut 32:26, 27
Eze 7:4

h 2Nya 36:17

i Kut 12:23
Yos 2:17-19
Ufu 9:4

j 2Fa 25:18, 21
Yer 25:29

wa na silaha yake ya kuangamiza mkononi mwake!”

2 Nikaona wanaume sita wakija kutoka upande wa lango la juu^a linalotazama kaskazini, kila mmoja akiwa na silaha yake ya kuponda mkononi mwake; na kulikuwa na mwanamume mmoja kati yao aliyevaa kitani, akiwa na kidau cha wino cha mwandishi kiunoni,^{*} nao wakaingia ndani na kusimama kando ya madhabahu ya shaba.^b

3 Kisha utukufu wa Mungu wa Israeli^c ukainuka kutoka mahali ulipokuwa umetulia juu ya makerubi na kwenda kwenye kizingiti cha mlango wa nyumba hiyo,^d naye akaanza kumwita kwa sauti yule mwanamume aliyevaa kitani, ambaye alikuwa na kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. **4** Yehova akamwambia: “Pita kotekote jijini, katika jiji lote la Yerusalemu, nawe uya-tie alama mapaji ya nyuso za watu wanaolia kwa uchungu na kwa maumivu makali^e kwa sababu ya mambo yote yanayochukiza yanayofanywa jijini.”^f

5 Naye akawaambia wale wengine huku nikisikia: “Pite-ni kotekote jijini baada yake na kua. Jicho lenu lisisikitike, wala msiwe na huruma hata kidogo.^g **6** Mnapaswa kuwau wote kabisa, mzee, kijana, bikira, mtoto mdogo, na wanawake.^h Lakini msimkaribie mtu yeyote aliye na ile alama.ⁱ Mnapaswa kuanzia mahali pangu patakati-fu.”^j Kwa hiyo wakaanza na wale wazee waliokuwa mbele

9:2 *Au “chombo cha kuweka wino cha mwandishi.”

ya ile nyumba.^a **7** Kisha aka-waambia: “Itieni nyumba una-jisi na kuzijaza nyua wale wa-liouawa.^b Nendeni!” Basi wa-kaenda na kuwaua watu jijini.

8 Walipokuwa wakiwaua, nilibaki mimi peke yangu, nikaanguka kifudufudi na kupaza sauti: “Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Je, utawaangamiza Waisraeli wote wanaobaki unapolimwagia ghadhabu yako jiji la Yerusalemu?”^c

9 Basi akaniambia: “Kosa la watu wa nyumba ya Israel ni Yuda ni kubwa sana, kubwa kwelikweli.^d Nchi imejaa umwagaji wa damu,^e nalo jiji limejaa ufasidi.^f Kwa maana wanasema, ‘Yehova ameiacha nchi hii, na Yehova haoni.’^g **10** Lakini mimi, jicho langu halitasikitika; wala sitawahurumia.^h Nitawaletea madhara ya njia yao juu ya kichwa chao wenyewe.”

11 Ndipo nikamwona yule mwanamume aliyevaa kitani, ambaye alikuwa na kidau cha wino kiunoni, akirudi na ku-leta habari akisema: “Nimefanya kama ulivyoni amuru.”

10 Nilipokuwa nikitazama, niliona juu ya anga lili-likuwa juu ya vichwa vya makerubi kitu kama jiwe la yakuti kikitokea juu yao, nacho kilifanana na kiti cha ufalme.ⁱ **2** Kisha akamwambia yule mwanamume aliyevaa kitani: “Ingia katikati ya magurudumu yanayozunguka,^k chini ya makerubi, na ujaze mikono yako miwili makaa yanayowaka^l kutoka katikati ya makerubi na kuyarusha juu ya jiji.”^m Basi akaingia huku nikitazama.

SURA YA 9

a Eze 8:11

b Omb 2:21

c Mwa 18:23
Eze 11:13d 2Nya 36:14
Isa 1:4e 2Fa 21:16
Yer 2:34
Mt 23:30

f Eze 22:29

g Isa 29:15
Eze 8:12h Eze 5:11
Eze 7:4

SURA YA 10

i Isa 6:1
Eze 1:22, 26
Ufu 4:2, 3

j Eze 9:2

k Eze 1:16

l Eze 1:13

m 2Fa 25:8, 9

Safu ya 2

a Eze 1:27, 28
Eze 9:3b Kut 40:35
2Nya 5:13
Eze 43:5c Zb 29:3, 4
Eze 1:24
Yoh 12:28, 29

d Eze 1:13

e Eze 9:2

f Eze 1:8

g Eze 1:15-18

3 Makerubi walikuwa wamesimama upande wa kulia wa ile nyumba mwanamume huyo alipoingia, nalo wingu likajaa katika ua wa ndani. **4** Na utukufu wa Yehova^a ukainuka kutoka kwa makerubi mpaka kwenye kizingiti cha mlango wa nyumba hiyo, na hatua kwa hatua nyumba hiyo ikajaa wingu,^b na ua ulikuwa umejaa mwangaza wa utukufu wa Yehova. **5** Na sauti ya mabawa ya makerubi ilisikika katika ua wa nje, kama sauti ya Mungu Mweza-Yote anapozungumza.^c

6 Kisha akamwamuru hivi yule mwanamume aliyevaa kitani: “Chukua moto kutoka katikati ya magurudumu yanayozunguka, kutoka katikati ya makerubi,” naye akaingia na kusimama kando ya gurudumu. **7** Kisha mmoja wa makerubi akaunyoosha mkono wake kuelekea moto uliokuwa katikati ya makerubi.^d Akachukua kiasi fulani na kukiweka kwenye mikono miwili ya yule aliyevaa kitani,^e naye akauchukua na kwenda nje. **8** Makerubi walikuwa na kitu kilichofanana na mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao.^f

9 Nilipokuwa nikitazama, niliona magurudumu manne kando ya makerubi, gurudumu moja kando ya kila kerubi, na magurudumu hayo yalionekana yaking’aa kama jiwe la krisolito.^g **10** Kuhusu mwonekano wake, yote manne yalifanana, yalionekana kama gurudumu moja likiwa katikati ya gurudumu lingine. **11** Yaliposonga, yaliweza kwenda upande wote kati ya zile pande nne bila kugeuka,

kwa maana yalikuwa yakienda upande ambao kichwa kilitazama nayo yalienda bila ku-geuka. **12** Miili yao yote, mifongo yao, mikono yao, mabawa yao, na yale magurudumu, magurudumu ya wote wanne, yalijaa macho kila mahali.^a **13** Kuhusu yale magurudumu, nilisikia sauti ikiyaita, “Magurudumu yanayozunguka!”

14 Kila mmoja wao* alikuwa na nyuso nne. Uso wa kwanza ulikuwa uso wa kerubi, uso wa pili ulikuwa uso wa mwanadamu, wa tatu ulikuwa uso wa simba, na wa nne ulikuwa uso wa tai.^b

15 Na wale makerubi walikuwa wakiinuka—walikuwa viumbe hai walewale nilio-waona* kwenye mto Kebari^c—**16** na wale makerubi waliposonga, magurudumu yalikuwa yakisonga kando yao; na wale makerubi walipoinua juu mabawa yao ili yawe juu sana ya dunia, magurudumu hayo hayakuwa yakigeuka au kuondoka kando yao.^d **17** Waliposimama tuli, nayo yalisimama tuli; nao walipoinuka, yaliinuka pamoja nao, kwa maana roho iliyokuwa ikitenda katika wale viumbe hai* ilikuwa ndani ya magurudumu.

18 Kisha utukufu wa Yehova^e ukaondoka kwenye kizingiti cha mlango wa nyumba na kusimama tuli juu ya makerubi.^f **19** Sasa makerubi wakainua juu mabawa yao na kuinuka kutoka duniani huku nikitazama. Yale magurudumu pia yalikuwa kando yao walipoondoka. Wakasimama

10:14 *Yaani, kila kerubi. **10:15** *Tnn., “kilikuwa kile kiumbe hai nilichoona.” **10:17** *Tnn., “roho ya yule kiumbe hai.”

SURA YA 10

a Ufu 4:6, 8

b Eze 1:6, 10
Ufu 4:7

c Eze 1:3

d Eze 1:19-21

e Eze 1:27, 28

f Eze 9:3
Eze 10:4

Safu ya 2

a Eze 11:22

b Eze 1:1, 22

c Eze 1:8

d Eze 1:10

e Eze 1:12
Eze 10:11

SURA YA 11

f Eze 10:19

g Isa 1:23
Eze 22:27

h Eze 12:27

i Eze 24:3

j Eze 3:17
Eze 20:46
Eze 21:2

k 2Pe 1:21

katika kizingiti cha lango la mashariki la nyumba ya Yehova, na utukufu wa Mungu wa Israeli ulikuwa juu yao.^a

20 Hao ndio viumbe hai ni-liokuwa* nimeona chini ya Mungu wa Israeli kwenye mto Kebari,^b basi nikajua kwamba walikuwa makerubi. **21** Wote wanne walikuwa na nyuso nne, mabawa manne, na kitu kilichoonekana kama mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao.^c **22** Na nyuso zao zilikuwa kama nyuso nilizokuwa nimeona kando ya mto Kebari.^d Kila mmoja wao alikuwa akienda mbele moja kwa moja.^e

11 Na roho ikaniinua juu na kunileta kwenye lango la mashariki la nyumba ya Yehova, lango linalotazama mashariki.^f Hapo langoni niliona wanaume 25, na miongoni mwao kulikuwa na Yaazania mwana wa Azuri na Pelatia mwana wa Benaya, wakuu wa watu.^g **2** Kisha Yeye akaniambia: “Mwana wa binadamu, hawa ndio wanaume wanaopanga uovu na kutoa ushauri wa uovu katika* jiji hili. **3** Wanasema, ‘Je, huu si wakati wa kujenga nyumba?’^h Jiji* ni chungu cha kupikia,^{#i} na sisi ni nyama.’

4 “Basi tabiri dhidi yao. Tabiri, mwana wa binadamu.”ⁱ

5 Ndipo roho ya Yehova ika-ja juu yangu,^k naye akaniambia: “Waambie, ‘Yehova anasema hivi: “Mambo mliyosema ni sahihi, enyi watu wa

10:20 *Tnn., “Huyu ndiye kiumbe hai niliyekuwa.” **11:2** *Au “dhidi ya.” **11:3** *Yaani, jiji la Yerusalemu, ambamo Wayahudi walidhani watalindwa. [#]Au “chungu cha kupikia chenye mdomo mpana.”

nyumba ya Israeli, nami ninajua mnachofikiria.* **6** Mmewafanya wengi wafe katika jiji hili, nanyi mmezijaza barabara zake watu waliokufa.””^a **7** “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Maiti mlizotawanya jijini ndizo nyama, nalo jiji ni chungu cha kupikia.’^b Lakini ninyi wenyewe mtatolewa ndani yake.”

8 “Mmeuogopa upanga,^c nami nitauleta upanga dhidi yenu,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **9** ‘Nitawatoa ninyi ndani yake na kuwatia mikononi mwa watu wa nchi ya kigeni na kutekeleza hukumu dhidi yenu.’^d **10** Mtauawa kwa upanga.^e Nitawahukumu kwenye mpaka wa Israeli,^f nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^g **11** Jiji halitakuwa chungu chenu cha kupikia, nanyi hamtakuwa nyama iliyo ndani yake; nitawahukumu ninyi kwenye mpaka wa Israeli, **12** nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova. Kwa maana hamkuteembea katika masharti yangu wala kutenda hukumu zangu,^h bali mmetenda kulingana na hukumu za mataifa yanayowazunguka.””ⁱ

13 Mara tu nilipotabiri, Pelatia mwana wa Benaya akafa, nami nikaanguka chini kifudufudi na kulia kwa sauti: “Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Je, utawaangamiza Waisraeli wanaobaki?”^j

14 Neno la Yehova likanjia tena likisema: **15** “Mwa-

11:5 *Au “mambo yanayokuja katika roho yenu.”

SURA YA 11

a Eze 7:23
Eze 22:3, 4

b Eze 24:6

c Yer 38:19

d Yer 39:6, 7
Yer 52:24-27

e 2Fa 25:18-21
2Nya 36:17

f 2Fa 14:25
Yer 52:27

g Eze 6:13

h Eze 9:7
Ne 9:34

i Kum 12:29-31
2Nya 28:1, 3
Zb 106:34-36

j Eze 9:8

Safu ya 2

a 2Fa 24:14, 15
Yer 24:5

b Law 26:44

c Isa 11:11, 12
Yer 30:10, 11
Eze 34:13, 14
Amo 9:14, 15

d Eze 37:23

e Yer 24:7
Yer 31:33
Yer 32:39

f Zb 51:10
Eze 36:31

g Zek 7:12

h Eze 36:26

na wa binadamu, ndugu zako, ndugu zako walio na haki ya kukomboa, pamoja na watu wote wa nyumba ya Israeli, wameambiwa na wakaaji wa Yerusalemu, ‘Msimkaribie Yehova. Nchi ni yetu; tumepewa ili tuimiliki.’ **16** Kwa hiyo waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Ingawa nimewapeleka mbali sana miongoni mwa mataifa, nami nimewatawanya katika nchi hizo,^a baada ya muda mfupi nitakuwa kwao mahali patakatifu katika nchi ambazo wameenda.””^b

17 “Kwa hiyo waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Pia nitawakusanya ninyi kutoka kwa mataifa na kuwakusanya kutoka katika nchi ambazo mmetawanywa, nami nitawapa nchi ya Israeli.’^c **18** Nao watarudi huko na kuondoa humo vitu vyote vinavyochukiza na mazoea yote yanayochukiza.^d **19** Nami nitawapa moyo wenye umoja,^e nami nitatia roho mpya ndani yao;^f nami nitauondoa moyo wa jiwe katika miili yao^g na kuwapa moyo wa nyama,^h **20** ili watembee katika sheria zangu na kushika hukumu zangu na kuzitii. Kisha watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao.”

21 ““Lakini kwa wale ambao miyo yao imeazimia kuendelea kufanya mambo yao yanayochukiza na mazoea yao yanayochukiza, nitawaletea madhara ya njia yao juu ya kichwa chao,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

11:19 *Tnn., “moyo mmoja.” #Yaani, moyo ulio mwepesi kutii mwongozo wa Mungu.

22 Sasa wale makerubi wakayainua juu mabawa yao, na yale magurudumu yalikuwa karibu nao,^a na utukufu wa Mungu wa Israeli ulikuwa juu yao.^b 23 Kisha utukufu wa Yehova^c ukapanda kutoka jijini ukasimama juu ya mlima ulio upande wa mashariki wa jiji hilo.^d 24 Kisha roho ikaniinua juu—katika maono kupitia roho ya Mungu—na kunileta kwa watu walio uhamishoni huko Ukaldayo. Kisha maono niliyokuwa nimeyao-na yakatoweka. 25 Nami nikaanza kuwaambia watu walio uhamishoni mambo yote ambayo Yehova alikuwa amenionyesha.

12 Neno la Yehova likanijia tena likisema: 2 “Mwana wa binadamu, unaishi katika nyumba ya uasi. Wana macho ya kuona, lakini hawaoni, na masikio ya kusikia, lakini hawasikii,^e kwa maana wao ni nyumba ya uasi.^f 3 Nawe, mwana wa binadamu, jitayarishie mizigo ya kwenda uhamishoni. Kisha, mchana wakiwa wanatazama, unapaswa kwenda uhamishoni. Toka nyumbani kwako uende uhamishoni mahali pengine huku wakitazama. Labda wataona, ingawa wao ni nyumba ya uasi. 4 Wakati wa mchana toa mizigo yako iliyofungwa kwa ajili ya kwenda uhamishoni huku wakitazama, kisha jioni huku wakitazama, uondoke kama mtu anayepelekwa uhamishoni.^g

5 “Toboa shimo ukutani huku wakitazama, nawe ubebe mizigo yako na kupitia humo.^h 6 Beba mizigo yako begani huku wakikutazama, nawe uende nayo gizani. Ufu-

SURA YA 11

a Eze 1:19

b Eze 10:18, 19

c Eze 9:3

Eze 10:4

d Zek 14:4

SURA YA 12

e Isa 6:9, 10

Yer 5:21

Ro 11:8

f Eze 2:3, 5

g 2Nya 36:20

Yer 52:10, 11

h 2Fa 25:4

Safu ya 2

a Isa 8:18

Eze 4:3

Eze 24:24

b Yer 21:7

Eze 21:25

c Eze 24:24

d Yer 52:15

e 2Fa 25:4

Yer 39:4

f Yer 52:9

Eze 17:20, 21

g 2Fa 25:6, 7

Yer 34:3

Yer 52:11

Eze 17:16

h 2Fa 25:5

i Law 26:33

Yer 42:15, 16

nike uso wako ili usiweze kuona chini, kwa maana ninakufanya uwe ishara kwa watu wa nyumba ya Israeli.”^a

7 Nikafanya kama nilivyoa-mriwa. Nikaitoa mizigo yangu nje mchana kama mizigo ya kwenda uhamishoni, na jioni nikatoboa shimo ukutani kwa mkono. Na kulipokuwa na giza, nikachukua mizigo yangu, nikaibeba begani mbele ya macho yao.

8 Asubuhi neno la Yehova likanijia tena likisema: 9 “Mwana wa binadamu, je, watu wa nyumba ya Israeli, nyumba ya uasi, hawakukuuliza, ‘Unafanya nini?’ 10 Waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Tangazo hili linamhusu mkuu^b huko Yerusalemu na watu wote wa nyumba ya Israeli walio jijini.””

11 “Waambie, ‘Mimi ni ishara kwenu.^c Kama vile nilivyotenda, ndivyo watakavyotendewa. Watapelekwa uhamishoni, utekwani.^d 12 Mkuu aliye miongoni mwao atabeba mizigo yake begani na kuondoka kukiwa na giza. Atatoboa shimo ukutani na kuibeba mizigo yake kupitia humo.^e Ataufunika uso wake ili asione chini.’ 13 Nitautandaza wavu wangu juu yake, naye atakamatwa katika wavu wangu wa kuwindia.^f Kisha nitampeleka Babiloni, kwenye nchi ya Wakaldayo, lakini hataiona; naye atafia huko.^g 14 Na wote wa-naomzunguka, wasaidizi wake na wanajeshi wake, nitawatawanya pande zote;^h nami nitauchomoa upanga ili kuwakimbiza.ⁱ 15 Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapowatawanya miongoni

mwa mataifa na kuwatawanya katika nchi hizo. **16** Lakini nitawalinda watu wachache kati yao wasife kwa upanga, njaa kali, na ugonjwa hatari, ili wasimulie kuhusu mazoea yao yote yanayochukiza miongoni mwa mataifa ambamo watapelekwa; nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

17 Nalo neno la Yehova likanijia tena likisema: **18** “Mwana wa binadamu, unapaswa kula mkate wako ukitetemeka na kunywa maji yako ukifadhaika na kuhaingaika.^a **19** Waambie watu wa nchi, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anawaambia hivi wakaaji wa Yerusalemu katika nchi ya Israeli: “Watakula mkate wao kwa wasiwasi na kunywa maji yao kwa hofu, kwa maana nchi yao itakuwa ukiwa kabisa^b kwa sababu ya ukatili wa wale wote wanaokaa ndani yake.^c **20** Majiji yanayokaliwa yataharibiwa, na nchi itakuwa ukiwa;^d nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”^e

21 Nalo neno la Yehova likanijia tena likisema: **22** “Mwana wa binadamu, ni methali gani hii mliyo nayo katika Israeli, inayosema, ‘Siku zinanipita, na maono yote hayatimii?’^f **23** Kwa hiyo waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Nita-fanya msemo huo ukome, nao hawatautumia tena kama methali katika Israeli.”’ Lakini waambie, ‘Siku zimekaribia,^g na maono yote yatatimia.’ **24** Kwa maana hakutakuwa tena na maono ya uwongo au uaguzi* wa udanga-

12:24 *Au “ubashiri.”

SURA YA 12

a Law 26:26

b Isa 6:11
Zek 7:14

c Zb 107:33, 34
Yer 6:7

d Isa 64:10
Yer 25:9

e Eze 6:13

f Isa 5:19
Amo 6:3
2Pe 3:3, 4

g Yoe 2:1
Sef 1:14

Safu ya 2

a Yer 14:14
Omb 2:14
Eze 13:23

b Omb 2:17
Zek 1:6

c Yer 16:9
Hab 1:5

d Isa 5:19
Isa 28:15
2Pe 3:3, 4

SURA YA 13

e Mik 3:5
Sef 3:4

f Yer 14:14
Yer 23:16

g Yer 23:32

h Eze 22:30

i Isa 2:12
Yoe 1:15

nyifu katika nyumba ya Israeli.^a **25** “Kwa maana mimi, Yehova, nitasema. Neno lolote nitakalosema litafanywa bila kukawia zaidi.^b Katika siku zenu,^c enyi nyumba ya uasi, nitasema neno na kulitimiza,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

26 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **27** “Mwana wa binadamu, hivi ndivyo watu wa* Israeli wanavyosema, ‘Maono anayoona ni ya muda mrefu kutoka sasa, naye anatabiri kuhusu wakati ujao ulio mbali.’^d **28** Kwa hiyo waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Hakuna neno langu lolote litakalokawia; jambo lolote nitakalosema litafanywa,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.””

13 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, tabiri dhidi ya manabii wa Israeli,^e nawe uwaambie hivi wale wanaotunga unabii wao wenyewe:^{*f} ‘Sikieni neno la Yehova. **3** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Ole wao manabii wapumbavu, wanaoifuata roho yao wenyewe, ingawa hawajaona chochote!^g **4** Ewe Israeli, manabii wako wamekuwa kama mbweha katika magofu. **5** Hamtaenda mahali palipobomoka katika kuta za mawe ili kuzijenga upya kwa ajili ya watu wa nyumba ya Israeli,^h ili Waisraeli waendeleo kusimama vitani katika siku ya Yehova.”ⁱ **6** “Wameona maono ya uwongo na kutabiri uwongo, wale

12:27 *Tnn., “nyumba ya.” 13:2 *Au “wanaotabiri kutoka moyoni mwao wenyewe.”

wanaosema, 'Neno la Yehova ni,' wakati ambapo Yehova mwenyewe hajawatuma, nao wamengoja neno lao litimie.^a **7** Je, ninyi hamkuona maono ya uwongo, na kutabiri uwongo, mnaposema, 'Neno la Yehova ni,' wakati ambapo sijasema lolote?"

8 "Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: "Kwa sababu mmesema uwongo na maono yenu ni ya uwongo, mimi niko dhidi yenu,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."^b **9** Mko-no wangu uko dhidi ya manabii ambao maono yao ni ya uwongo na wanaotabiri uwongo.^c Nao hawatakuwa miongoni mwa watu ninao-wambia siri zangu; wala hawataandikwa katika orodha ya watu wa nyumba ya Israeli; wala hawatarudi katika nchi ya Israeli; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ndiye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.^d **10** Hayo yote ni kwa sababu wamewapotosha watu wangu wakisema, "Kuna amani!" wakati hakuna amani.^e Ukuta dhaifu unapojengwa, wanaupiga lipu kwa chokaa."^{*f}

11 "Waambie wale wanaopiga lipu kwa chokaa kwamba ukuta huo utaanguka. Mvua kubwa ya mafuriko itakuja, mvua ya mawe itanyesha,^{*} na dhoruba kali za upepo zitaubomoa.^g **12** Na ukuta huo utakapoanguka mtaulizwa, 'Chokaa mliyopaka iko wapi?'"^h

13 "Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Nitasababisha dhoru-

13:10 *Yaani, wanajenga ukuta wa ndani ulio dhaifu na kujaribu kuufanya uonekane imara kwa chokaa. **13:11** *Tnn., "nanyi, enyi mawe ya mvua mtanyesha."

SURA YA 13

a Yer 29:31, 32

b Eze 22:28

c Yer 14:14
Yer 28:15, 16
Yer 29:8, 9

d Eze 6:13
Eze 11:10

e Yer 6:13, 14

f Isa 30:10
Eze 22:28

g Isa 27:8

h Yer 37:19

Safu ya 2
a Isa 30:12, 13

b Yer 6:13, 14
Yer 28:1-4

ba kali za upepo zilipuke kwa ghadhabu yangu, na mvua kubwa ya mafuriko kwa hasira yangu, na mvua ya mawe kwa ghadhabu inayoangamiza. **14** Nitaubomoa ukuta ambao mmeupiga lipu kwa chokaa na kuuangusha chini ardhini, na msingi wake utafunuliwa. Jiji litakapoanguka, mtaangamia ndani yake; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.'

15 "Nitakapouwagia ukuta huo ghadhabu yangu yote na kuwamwagia wale waliou-piga lipu kwa chokaa, nita-waambia ninyi: "Ukuta hau-po tena, na wale wanaoupiga lipu hawapo tena."^a **16** Manabii wa Israeli hawapo tena, wale wanaowatabiria watu wa Yerusalemu na kuona maono ya amani kwa ajili yao, wakati hakuna amani,"^b asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

17 "Nawe, mwana wa binadamu, uelekeze uso wako dhidi ya mabinti wa watu wako wanaotunga unabii wao wenyewe, nawe utabiri dhidi yao.

18 Waambie, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: "Ole wao wanawake wanaoshona pamoja tepe kwa ajili ya mikono yote^{*} na kutengeneza shela kwa ajili ya vichwa vya kila ukubwa ili kuwinda uhai wa^u watu! Je, mnawinda uhai wa^u watu wangu na kujaribu kuhifadhi uhai wenu^u wenyewe? **19** Je, mtanitia unajisi miongoni mwa watu wangu kwa ajili ya makonzi ya shayiri na kwa ajili ya makombo

13:18 *Yaani, tepe za uchawi zinazovaliwa kwenye viwiko au mkononi. ^aAu "nafsi za." ^uAu "nafsi za." ^uAu "nafsi zenu."

ya mkate,^a mkiwaua watu wasiostahili kufa na kuwacha hai watu wasiostahili kuisi, kwa kuwadanganya watu wangu, wanaosikiliza uwongo wenu?”^b

20 “Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Niko dhidi ya tepe zenu enyi wanawake, mnazotumia kuwinda watu* kana kwamba wao ni ndege, nami nitazirarua kutoka mikononi mwenu na kuwafungua watu mnaowawinda kama ndege. **21** Nitazirarua shela zenu na kuwako koa watu wangu kutoka mikononi mwenu, nao hawatakuwa tena windo lenu; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^c **22** Kwa sababu mmemvunja moyo aliye mwadilifu kwa uwongo wenu^d ingawa mimi mwenyewe si kuwa nimemsababishia taabu,* nanyi mmeimarisha mikono ya mwovu^e ili asiache njia yake ya uovu na kuendelea kuishi.^f **23** Kwa hiyo, ninyi wanawake hamtaona tena maono ya uwongo na kufanya uaguzi;^g nami nitawako koa watu wangu kutoka mikononi mwenu, nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’”

14 Na baadhi ya wazee wa Israeli wakaja na kuketi mbele yangu.^h **2** Kisha neno la Yehova likanijia likisema: **3** “Mwana wa binadamu, wanaume hawa wameazimia kufuata sanamu zao zinazochukiza,* nao wameweka kikwazo kinachowafanya

13:20 *Au “nafsi.” 13:22 *Au “maumivu.” 13:23 *Au “ubashiri.” 14:3 *Hue nda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

SURA YA 13

a Mik 3:11

b Yer 23:14

c Eze 6:13

d Yer 27:14

e Yer 23:14

f Yer 23:16, 17

g Kum 18:10, 14
Yer 27:9
Mik 3:6

SURA YA 14

h Eze 33:30, 31

Safu ya 2

a 2Fa 3:13
Isa 1:15
Yer 11:11

b Yer 2:5

c Isa 55:7

d Yer 21:1, 2
Eze 33:31

e Law 20:2, 3

watu watende dhambi. Je, ni waruhusu waniombe ushauri?^a **4** Sasa zungumza nao uwaambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Ikiwa Mwisraeli ameazimia kufuata sanamu zake zinazochukiza na kuweka kikwazo kinachowafanya watu watende dhambi kisha anaenda kuomba ushauri kutoka kwa nabii, mimi, Yehova, nitamjibu ipasavyo kulingana na sanamu zake nyingi zinazochukiza. **5** Kwa maana nitatia hofu katika mioyo ya watu wa nyumba ya Israeli* kwa sababu wote wameniacha na kuzifuata sanamu zao zinazochukiza.’”^b

6 “Basi waambie watu wa nyumba ya Israeli, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Rudini na mziache sanamu zenu zinazochukiza na mgeuze nyuso zenu kutoka kwenye mazoea yenu yanayochukiza.^c **7** Kwa maana ikiwa Mwisraeli yeyote au mgeni anayeishi Israeli anajitenga nami na kuazimia kufuata sanamu zake zinazochukiza na kuweka kikwazo kinachowafanya watu watende dhambi, kisha aje kuomba ushauri kutoka kwa nabii wangu,^d mimi, Yehova, nitamjibu mimi mwenyewe. **8** Nitamkataa* mtu huyo na kumfanya awe ishara ya kuonya na methali, nami nitamwangamiza kabisa kutoka kati ya watu wangu;^e nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’”

9 “‘Lakini nabii akipumbazwa naye atoe ushauri, ni mimi, Yehova, ambaye nime-

14:5 *Tnn., “nitawakamata watu wa nyumba ya Israeli katika moyo wao.” 14:8 *Tnn., “Nitaukaza uso wangu dhidi ya.”

mpumbaza nabii huyo.^a Ndi-po nitakapounyoosha mkono wangu dhidi yake na kumwangamiza kutoka kwa watu wangu Waisraeli. **10** Nao lazima wataibeba hatia yao; hatia ya mwenye kuomba ushauri itakuwa sawa na hatia ya nabii, **11** ili watu wa nyumba ya Israeli waache kutangatanga mbali nami na kuacha kujichafua kwa makosa yao yote. Nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao,^b asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

12 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **13** “Mwana wa binadamu, ikiwa nchi itanitendea dhambi kwa kukosa uaminifu, nitaunyoosha mkono wangu dhidi yake na kufanya chakula kisipatikane^{*c} na kuleta njaa kali nchini^d na kuwaangamiza kabisa wanadamu na wanyama kutoka humo.”^e **14** “Hata ikiwa watu hawa watatu—Noa,^f Danieli,^g na Ayubu^h—wangekuwa humo, wangejiokoa wao wenyewe* tu kwa sababu ya uadilifu wao,ⁱ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

15 “Au nikifanya wanyama hatari wa mwituni wapite kotekote nchini na kuwaua watu wengi* na kuifanya nchi iwe ukiwa hivi kwamba hakuna mtu atakayepita humo kwa sababu ya wanyama wa mwituni,^j **16** kama ninavyoishi,^k asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘hata ikiwa watu hao watatu wangekuwa humo,

14:13 *Tnn., “kuvunja fito zake za mikate.” Labda ni fito zilizotumiwa kuhifadhia mikate. **14:14** *Au “wangeokoa nafsi zao.” **14:15** *Au “na kuwaua watoto.”

SURA YA 14

a 1Fa 22:21, 22
Yer 4:10
2Th 2:10, 11

b Yer 24:7
Eze 11:19, 20

c Law 26:26

d Isa 3:1
Yer 15:2

e Yer 7:20

f Mwa 6:8, 9
Ebr 11:7

g Da 10:11

h Ayu 1:8
Ayu 42:8

i Met 11:4
Yer 15:1
2Pe 2:9

j Law 26:22
Yer 15:3

Safu ya 2

a Law 26:25
Yer 25:9
Eze 21:3

b Sef 1:3

c Kum 28:21, 22

d Mwa 7:1

e Da 10:11

f Ayu 1:8
Ayu 42:8

g Eze 18:20
Sef 2:3

h Yer 15:2

i Eze 5:17
Eze 33:27

j Yer 32:43

k Kum 4:31
2Nya 36:20
Eze 6:8
Mik 5:7

hawangewaokoa wana wao wala mabinti wao; wangejiokoa wao wenyewe tu, na nchi ingekuwa ukiwa.”

17 “Au kama nikileta upanga dhidi ya nchi hiyo^a na kusema: “Upanga na upite kotekote nchini,” na kuwaangamiza wanadamu na wanyama kutoka humo,^b **18** hata ikiwa watu hao watatu wangekuwa humo, kwa hakika kama ninavyoishi,^c asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘hawangewaokoa wana wao wala mabinti wao; wangejiokoa wao wenyewe tu.”

19 “Au nikileta ugonjwa hatari katika nchi hiyo^c na kuimwagia ghadhabu yangu kwa umwagaji wa damu ili kuwaangamiza wanadamu na wanyama kutoka humo, **20** hata ikiwa Noa,^d Danieli,^e na Ayubu^f wangekuwa humo, kwa hakika kama ninavyoishi,^g asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘hawangewaokoa wana wao wala mabinti wao; wangejiokoa wao wenyewe tu kwa sababu ya uadilifu wao.”^g

21 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Ndivyo itakavyokuwa nitakapoleta adhabu zangu nne^{*h}—upanga, njaa kali, wanyama hatari wa mwituni, na ugonjwa hatari—dhidi ya jiji la Yerusalemu ili kuwaangamiza kabisa wanadamu na wanyama kutoka humo.^j **22** Lakini, baadhi ya watu waliobaki humo wataponyoka na kutolewa nje,^k wana na mabinti. Wanakuja kweni, nanyi mtakapoona njia

14:21 *Au “matendo yangu manne ya hukumu yanayodhuru.”

zao na matendo yao, kwa hakika mtafarijiwa kuhusiana na msiba ambao nilileta dhidi ya Yerusalemu, kuhusu kila jambo ambalo nilitenda dhidi ya jiji hilo.”

23 “Watawafariji mtakaopona njia zao na matendo yao, nanyi mtajua kwamba sikutenda bila sababu yale niliyolazimika kulitendea jiji hilo,^a asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

15 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, mbao za mzabibu hutofautianaje na za mti mwingine wote au tawi la miti ya msituni? **3** Je, ufito wake unaweza kutumiwa kufanyia kazi? Au je, watu huutumia kuteengeneza kijiti cha kuning’ini zia vyombo? **4** Tazama! Hutupwa motoni uwe kuni, na moto huchoma miisho yote miwili na kuunguza katikati. Je, sasa unafaa kwa kazi yoyote? **5** Hata ulipokuwa mzima, haungetumiwa kwa chochote. Je, utakuwa na thamani yoyote baada ya kuchomwa na kuunguzwa na moto?”

6 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kama mbao za mzabibu kati ya miti ya msituni, ambazo nimezitoa ziwe kuni kwa ajili ya moto, ndivyo nitakavyoshughulika na wakaaji wa Yerusalemu.^b **7** Nimewakataa.* Wameponyoka kutoka motoni, lakini moto utawateketeza. Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapowakataa.’”^{#c}

15:7 *Tnn., “Nimeukaza uso wangu dhidi yao.” #Tnn., “nitakapoukaza uso wangu dhidi yao.”

SURA YA 14

a Ne 9:33
Yer 22:8, 9
Eze 9:9
Da 9:7

SURA YA 15

b Zb 80:14-16
Isa 5:24
Yer 7:20
Eze 20:47

c Eze 6:7
Eze 7:4

Safu ya 2

a Isa 6:11
Yer 25:11
Eze 6:14

b 2Nya 36:14

SURA YA 16

c Eze 8:10
Eze 20:4

d Yos 10:5
1Fa 21:25, 26
2Fa 21:11

e 1Nya 1:13, 14

8 “‘Nami nitaifanya nchi iwe ukiwa^a kwa sababu wame-tenda kwa ukosefu wa uaminifu,’^b asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

16 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, lijulisho Yerusalemu mazoea yake yanayochukiza.^c **3** Nawe utaliambia, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anakuambia hivi Yerusalemu: ‘Asili yako na kuzaliwa kwako ni katika nchi ya Mkanaani. Baba yako alikuwa Mwamori,^d na mama yako alikuwa Mhiti.^e **4** Kuhusu kuzaliwa kwako, siku uliyozaliwa, kitovu chako hakikukatawa, hukuoshwa kwa maji uwe safi, hukusuguliwa kwa chumvi, wala hukufungwa kwa vitambaa. **5** Hakuna mtu aliyekusikitikia vya kutosha hivi kwamba akakufanyia lolote kati ya mambo hayo. Hakuna mtu aliyekuhurumia. Badala yake, ulitupwa uwanjani kwa sababu ulichukiwa* siku uliyozaliwa.

6 “‘Nilipokuwa nikipita, nilikuona ukitupatupa mateke katika damu yako, nawe ulipokuwa umelala hapo katika damu yako, nikasema: ‘Endelea kuishi!’ Naam, nilikuaambia ukiwa umelala hapo katika damu yako: ‘Endelea kuishi!’ **7** Nilikufanya uwe umati mkubwa sana, kama mimea inayochipuka shambani, nawe ukakua, ukakomaa na kuvaa mapambo bora sana. Matiti yako yakakomaa, na nywele zako zikakua; lakini bado ulikuwa uchi, bila chochote.”

8 “‘Nilipokuwa nikipita na kukuona, nilitambua kwamba

16:5 *Au “nafsi yako ilichukiwa.”

ulikuwa na umri wa kutosha kuonyeshwa upendo. Basi nikatandaza vazi langu juu yako^a na kuufunika uchi wako, nami nikaapa na kufanya agano pamoja nawe,^e asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘nawe ukawa wangu. **9** Isitoshe, nilikuosha kwa maji na kuiondoa damu iliyo-kuwa juu yako na kukupaka mafuta.^b **10** Kisha nikakuvika vazi lililotariziwa na kukupa viatu vya ngozi bora* na kukufunika kwa kitani bora, nami nikakuvika mavazi ya bei ghali. **11** Nikakupamba kwa vito na kutia bangili kwenye mikono yako na mkufu shingoni mwako. **12** Pia nikatia pete ya puani kwenye pua yako na vipuli kwenye masikio yako na taji maridadi kwenye kichwa chako. **13** Ukaendelea kujipamba kwa dhahabu na fedha, na mavazi yako yalikuwa kitani bora, kitambaa cha bei ghali, na vazi lililotariziwa. Uliku- la unga laini, asali, na mafuta, nawe ukawa mrembo kupindukia,^c ukastahili kuwa malkia.”*

14 “Sifa zako zikaanza* kuenea kati ya mataifa^d kwa sababu ya urembo wako, kwa maana urembo wako ulikuwa kamili kwa sababu niliweka fahari yangu mwenyewe juu yako,^e asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

15 “Lakini ulianza kuumtumi ulianza urembo wako,^f nawe ukawa kahaba kwa sababu ya sifa zako.^g Ulimmwagia kila mpita-njia matendo

16:10 *Au “ngozi ya sili.” **16:13** *Au “ukastahili cheo cha kifalme.” **16:14** *Au “Jina lako likaanza.”

SURA YA 16

a Ru 3:9

b Zb 23:5

c Zb 48:2

d 1Fa 4:21

e 1Fa 10:1
Zb 50:2
Omb 2:15

f Yer 7:4
Mik 3:11

g 1Fa 11:5, 7
Zb 106:35, 36
Isa 57:7, 8
Yer 2:20
Yak 4:4

Safu ya 2

a Yer 3:13

b 1Fa 14:22, 23
2Nya 21:5, 11

c Isa 57:7, 8

d Eze 8:10, 11

e 2Fa 22:16, 17

f Kut 13:2

g Zb 106:37, 38

h Law 18:21
Law 20:2
2Fa 16:1, 3
2Nya 33:1, 6
Yer 7:31
Eze 20:26

i Yer 13:27
Sef 3:1

yako ya ukahaba,^a na urembo wako ukawa wake. **16** Uka- chukua baadhi ya mavazi yako na kutengeneza mahali pa juu penye rangi mbalimbali ambapo ulifanyia ukahaba^b—mambo hayo hayapaswi kufanywa, wala hayapaswi kutendeka kamwe. **17** Pia, ulichukua vito vyako maridadi vilivyotengenezwa* kwa dhahabu na fedha ambayo nilikupatia nawe ukajite- ngenezea sanamu za kiume na kufanya nazo ukahaba.^c **18** Nawe ukachukua mavazi yako yaliyotariziwa na kuzifunika,^e nawe ukazitolea mafuta yangu na uvumba wangu.^d **19** Na mkate wangu nilikuwa nimekupa—uliotenge- nezwa kwa unga laini, mafuta, na asali niliyokupa ule—uliu- toa pia kwa sanamu hizo ukiwa harufu inayopendeza.*^e Hivyo ndivyo ilivyokuwa,^e asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

20 “Uliwachukua wana na mabinti wako uliokuwa ume- nizalia,^f nawe ukawatoa dha- bihu kwa sanamu hizo ili waangamizwe^g—je, matendo yako ya ukahaba hayajato- sha? **21** Uliwachinja wana- ngu, nawe ukawatoa wawe dhabihu kwa kuwateketeza* motoni.^h **22** Ulipokuwa uki- tenda mambo yako yote yana- yochukiza na matendo ya ukahaba, hukukumbuka siku za ujana wako ulipokuwa uchi, bila chochote, ukitupatupa mateke katika damu yako. **23** Baada ya uovu wako wote, ole, ole wako,ⁱ asema

16:17 *Au “mapambo yako maridadi ya- liyotengenezwa.” **16:18** *Yaani, sanamu za kiume. **16:19** *Au “inayotuliza.” **16:21** *Tnn., “kuwapitisha.”

Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **24** ‘Ulijijengea kilima na kujitengenezea mahali pa juu katika kila kiwanja cha jiji. **25** Ulijenga mahali pako pa juu sehemu zinazoonekana zaidi za kila barabara, nawe ukageuza urembo wako kuwa kitu kinachochukiza kwa kuutoa mwili wako* kwa kila mpita-njia,^a nawe ukazidisha matendo yako ya ukahaba.^b **26** Ulifanya ukahaba na wana wa Misri,^c majirani wako wenye uchu,^{*} nawe ulinikasirisha kwa matendo yako yasiyohesabika ya ukahaba. **27** Sasa nitauleta mkono wangu dhidi yako na kupunguza posho yako ya chakula^d na kukutia mikononi mwa mapeenzi* ya wanawake wanaokuchukia,^e mabinti wa Wafilisti, wanawake walioshtushwa na mwenendo wako mchafu.^f

28 “Kwa kuwa hungeweza kutoshelezwa, ulifanya pia ukahaba na wana wa Ashuru,^g lakini baada ya kufanya nao ukahaba, bado hukutosheka. **29** Basi ukazidisha ukahaba wako kuelekea nchi ya wafanyabiashara* na kuelekea kwa Wakaldayo,^h lakini bado hukutosheka. **30** Jinsi moyo wako ulivyokuwa mgonjwa,^{*} asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘ulipofanya mambo hayo yote, ukitenda kama kahaba mwenye ushupavu!’ **31** Lakini ulipojenga kilima chako katika sehemu

16:25 *Tnn., “kupanua miguu yako.”
16:26 *Tnn., “majirani wako wenye mwili mkubwa.” 16:27 *Au “nafsi.” 16:29 *Tnn., “nchi ya Kanaani.” 16:30 *Au “Jinsi moyo wako ulivyokuwa dhaifu.” Au labda, “Jinsi nilivyojawa na ghadaha dhidi yako.”

SURA YA 16

a Yer 2:23, 24

b Yer 3:2

c Isa 30:2, 3
Yer 2:36

d Kum 28:48

e Zb 106:41

f Yer 2:11, 12

g 2Fa 16:7

h Eze 23:14, 16

i Yer 3:3

Safu ya 2

a Yer 3:1, 20

b Mwa 38:16

c Isa 57:9

d 2Nya 16:2, 3

e Isa 1:21
Yer 3:6

f 2Fa 21:11

g Zb 106:37, 38

h Yer 13:22
Omb 1:8i Mwa 38:24
Law 20:10
Kum 22:22j Mwa 9:6
Kut 21:12

zinazoonekana zaidi za kila barabara na kutengeneza mahali pako pa juu katika kila kiwanja cha jiji, hukuwa kama kahaba, kwa sababu ulikataa malipo yoyote. **32** Wewe ni mke mzinzi anayewachukua wageni badala ya mume wake mwenyewe!^a **33** Watu huwapa zawadi makahaba wote,^b lakini wewe ndiye unayewapa zawadi wote walio na uchu kuelekea,^c nawe unawapa rushwa ili waje kwako kutoka pande zote ili kufanya ukahaba.^d **34** Wewe ni tofauti kabisa na wanawake wengine wanaofanya ukahaba. Hakuna mtu anayefanya ukahaba kama wewe! Unawalipa watu, nao hawakulipi. Unatenda tofauti kabisa.^e

35 “Kwa hiyo, ewe kahaba,^e sikia neno la Yehova. **36** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu uchu wako umemwagwa na uchi wako umefunuliwa ulipokuwa ukifanya ukahaba na wapenzi wako na sanamu zako zote zinazoudhi na kuchukiza* ambazo hata ulizitolea dhabihu ya damu ya wanao,^g **37** kwa hiyo ninawakusanya pamoja wapenzi wote ambao umewapa raha, wote uliowapenda na wote uliowachukia. Nitawakusanya pamoja dhidi yako kutoka pande zote na kuwafunulia uchi wako, nao watakuona ukiwa uchi kabisa.^h

38 “‘Nami nitakuadhibu kwa hukumu wanayostahili wanawake wazinziⁱ na wanawake wanaomwaga damu,^j na damu

16:36 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

yako itamwagwa kwa ghadhabu na wivu.^a **39** Nitakutia mikononi mwao, nao watavibomoa vilima vyako, na mahali pako pa juu patabomolewa;^b nao watakuvuva mavazi yako^c na kuchukua vito vyako* maridadi^d na kukuacha uchi, bila chochote. **40** Wataleta umati dhidi yako,^e nao watakupiga mawe^f na kukuchinja kwa panga zao.^g **41** Watazitekeleza nyumba zako kwa moto^h na kutekeleza hukumu dhidi yako mbele ya macho ya wanawake wengi; nami nitakomesha ukahaba wako,ⁱ nawe utaacha kutoa malipo. **42** Nitaitosheleza ghadhabu yangu dhidi yako,^j na hasira yangu itakuacha;^k nami nitatulia na sitaendelea kukasirika.^l

43 “Kwa sababu hukuzikumbuka siku za ujana wako^l nawe umenikasirisha kwa kufanya mambo hayo yote, sasa nitakuletea madhara ya njia zako juu ya kichwa chako mwenyewe,^m asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘nawe hutaendelea tena na mwenendo wako mchafu na mazoea yako yote yanayochukiza.’

44 “Tazama! Kila mtu anayetumia methali ataitumia methali hii kukuhusu: “Kama mama alivyo, ndivyo binti alivyo!”^m **45** Wewe ni binti ya mama yako, aliyemdharau mume wake na watoto wake. Nawe ni dada ya dada zako, waliowadharau waume zao na watoto wao. Mama yenu alikuwa Mhiti, na baba yenu alikuwa Mwamori.”ⁿ

46 “Dada yako mkubwa ni

16:39 *Au “mapambo yako.”

SURA YA 16

a Zb 79:2, 3

Eze 23:25

b Isa 27:9

Eze 16:24

c Yer 4:30

d Isa 3:18-23

Eze 23:26

e Eze 23:46, 47

Hab 1:6

f Kum 22:20, 21

g 2Nya 36:17

Yer 25:9

h 2Fa 25:8, 9

i Eze 23:27

j Eze 5:13

k Isa 40:2

l Yer 2:32

m 1Fa 21:25, 26

2Fa 21:2, 9

Zb 106:35, 36

n Kum 20:17

Yos 10:5

2Fa 21:11

Eze 16:3

Safu ya 2

a Eze 23:33

b Yer 3:8

c Mwa 18:20

Isa 3:9

Yer 23:14

d Mwa 19:24, 25

e 2Fa 21:2, 9

Eze 5:5, 6

f Yud 7

g Met 16:5

h Mwa 13:10

i Met 1:32

j Met 21:13

k Met 16:18

l Mwa 13:13

Mwa 18:20

Mwa 19:4, 5

m Mwa 19:24, 25

Omb 4:6

2Pe 2:6

n 2Fa 21:13

Yer 23:13

Eze 23:33

o Yer 3:11

Samaria,^a anayekaa upande wako wa kaskazini* pamoja na mabinti zake,^{#b} na dada yako mdogo, anayekaa upande wako wa kusini,[^] ni Sodoma^c pamoja na mabinti zake.^d **47** Hukutembea tu katika njia zao na kufuata mazoea yao yanayochukiza, bali pia kwa muda mfupi mwenendo wako ulikuwa mpotovu hata zaidi kuliko mwenendo wao.^e **48** Kwa hakika kama ninavyoishi,[’] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘Sodoma dada yako na mabinti zake hawajatenda yale ambayo wewe na mabinti zako mmetenda. **49** Tazama! Hili ndilo lililokuwa kosa la Sodoma dada yako: Yeye pamoja na mabinti zake^f walikuwa na kiburi,^g nao walikuwa na chakula kingi^h na utulivu mwingi;ⁱ hata hivyo hawakuwasaidia walioteseka na maskini.^j **50** Waliendelea kuwa na majivuno^k na kuzidi kutenda mambo yanayochukiza machoni pangu,^l basi nikalazimika kuwaondoa.^m

51 “Samariaⁿ hata haku-tenda nusu ya dhambi zako. Uliendelea kuzidisha mazoea yako yanayochukiza kuliko yao, hivi kwamba dada zako wakaonekana kuwa waadilifu kwa sababu ya mazoea yako yote yanayochukiza.^o **52** Lazima sasa ubebe fedheha yako kwa kuwa umetee* tabia za dada zako. Kwa sababu ya dhambi yako ya kute-nda mambo yanayochukiza kuliko wao, wao ni waadilifu kuliko wewe. Basi sasa, na

16:46 *Tnn., “upande wako wa kushoto.”
#Labda ni miji ya jiji hilo. ^Tnn., “upande wako wa kulia.” 16:52 *Au “umeungu mkono.”

uaibike na kubeba fedheha ya kuwafanya dada zako waonekane kuwa waadilifu.’

53 “Nami nitawakusanya watu wao waliotekwa, watu waliotekwa wa Sodoma pamoja na mabinti zake na watu waliotekwa wa Samaria pamoja na mabinti zake; na pamoja nao nitawakusanya pia watu wako waliotekwa,^a **54** ili uibebe fedheha yako; nawe utafedheheka kwa sababu ya yale ambayo umefanya kwa kuwafariji. **55** Na dada zako wewe mwenyewe, Sodoma na mabinti zake, watarudia hali yao ya mwanzoni, na Samaria na mabinti zake watarudia hali yao ya mwanzoni, na wewe pamoja na mabinti zako mtarudia hali yenu ya mwanzoni.^b

56 Dada yako Sodoma haku-stahili kutajwa nawe katika siku ya fahari yako, **57** kabla uovu wako mwenyewe haujafunuliwa.^c Sasa mabinti wa Siria na majirani zake wanakushutumu, na mabinti wa Wafilisti,^d wote wanaokuzunguka, wanakudharau. **58** Utayabeba madhara ya mwenendo wako mchafu na mazoea yako yanayochukiza,’ asema Yehova.”

59 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Sasa nitakutendea kama ulivyotenda,^e kwa maana ulikidharau kiapo kwa kuvunja agano langu.^f **60** Lakini mimi mwenyewe nitalikumbuka agano nililofanya pamoja nawe katika siku za ujana wako, nami nitafanya agano la kudumu pamoja nawe.^g **61** Utakumbuka tabia yako na kufedheheka^h utakapowakaribisha dada zako,

SURA YA 16

a Zb 126:1

b Eze 36:11

c Eze 21:24

d 2Nya 28:18

e Isa 3:11
Gal 6:7

f Kum 29:12
Yer 22:8, 9

g Yer 32:40
Yer 50:4, 5

h Eze 20:43

Safu ya 2

a Ezr 9:6
Eze 36:31

b Zb 103:12
Mik 7:18, 19

SURA YA 17

c Ho 12:10

d Kum 28:49, 50
Yer 4:13
Omb 4:19

e Yer 22:23

f 2Fa 24:12
2Nya 36:9, 10
Yer 24:1

g 2Fa 24:15

h 2Fa 24:17
Yer 37:1

i Eze 17:13, 14

j 2Nya 36:11

waliokuzidi umri na pia walio na umri mdogo kuliko wako, nami nitakupa wawe mabinti zako, lakini si kwa sababu ya agano lako.’

62 “Na mimi mwenyewe nitafanya agano langu pamoja nawe; nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova. **63** Kisha utakumbuka na kuaibika sana usiweze kuufungua mdomo wako kwa sababu ya kufedheheka,^a nitakapofunika dhambi zako licha ya mambo yote ambayo umefanya,^b asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

17 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, tega kitendawili na useme methali kuhusu watu wa nyumba ya Israeli.^c **3** Nawe utasema, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Tai mku-bwa,^d mwenye mabawa maku-bwa, na manyoya marefu, na aliyejaa manyoya yenye rangi mbalimbali, alikuja Lebanoni^e na kuchukua sehemu ya juu ya mwerezi.^f **4** Aliling’oa chipukizi lake lililo juu zaidi na kulileta kwenye nchi ya wafanyabiashara* na kuliweka katika jiji la wafanyabiashara.^g **5** Kisha akachukua baadhi ya mbegu za nchi hiyo^h na kuziweka katika shamba lenye rutuba. Akaipanda mbe-gu moja kama mti wa mvinje kando ya maji mengi. **6** Basi ikachipuka na kuwa mzabibu mfupi, unaotambaa,ⁱ wenyewe majani yanayotazama ndani na mizizi inayokua chini yake. Kwa hiyo ukawa mzabibu, ukatokeza machipukizi na kuota matawi./

17:4 * Tnn., “nchi ya Kanaani.”

7 “Akaja tai mwingine mkubwa,^a mwenye mabawa makubwa na manyoya maku-bwa.^b Kisha mzabibu huo ukasambaza mizizi yake kwa bidii kumwelekea, mbali na bustani mahali ambapo ulipandwa, nao ukaelekeza majani yake kwake ili aumwagilie maji.^c 8 Ulikuwa tayari umepandwa katika shamba zuri karibu na maji mengi, ili utokeze matawi, uzae matunda, na uwe mzabibu mkubwa.”^d

9 “Sema, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Je, utasitawi? Je, mtu fulani hataing’oa mizizi yake^e na kufanya matunda yake yaoze na machipukizi yake yanauke?’^f Utakauka sana hivi kwamba hautahitaji mkono wenye nguvu wala watu wengi ili kuung’oa pamoja na mizizi yake. 10 Ingawa umepandikizwa, je, utasitawi? Je, hautakauka kabisa, utakapopi-gwa na upepo wa mashariki? Utakauka katika bustani uli-kochipuka.””

11 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: 12 “Tafadhali iambie nyumba ya uasi, ‘Je, hamtambui maana ya mambo haya?’ Sema, “Tazama! Mfalme wa Babiloni alikuja Yerusalemu, akamchukua mfalme wake na wakuu wake na kurudi pamoja nao Babiloni.^g 13 Isitoshe, alimchukua mmoja aliyekuwa wa uzao wa^h kifalme, akafanya naye agano na kumwapisha.ⁱ Kisha akawachukua watu mashuhuri wa nchi,^j 14 ili ufalme huo ushushwe, usiweze kuinuka, ili uendelee kuwapo ikiwa tu utashika agano lake.^k 15 Laki-

17:13 *Tnn., “mbegu ya.”

SURA YA 17

a Eze 17:15

b Yer 37:5, 7

c 2Fa 24:20
2Nya 36:11, 13

d Yer 37:1

e Yer 21:7

f 2Fa 25:7

g 2Fa 24:12, 14
Isa 39:7
Yer 22:24, 25
Yer 52:31, 32

h 2Fa 24:17
Yer 37:1

i 2Nya 36:11, 13

j 2Fa 24:15
Yer 24:1

k Yer 27:12
Yer 38:17

Safu ya 2

a 2Fa 24:20
2Nya 36:11, 13

b Kum 17:16

c Yer 37:5

d Yer 32:3, 4

e Yer 34:2, 3
Yer 52:11

f Yer 37:7, 8
Omb 4:17
Eze 29:6

g Kum 5:11

h Eze 12:13

i Eze 20:36

ni mwishowe mfalme huyo alimwasi^a kwa kutuma wajumbe wake Misri ili apate farasi^b na jeshi kubwa kutoka huko.^c Je, atafanikiwa? Je, yule anayefanya mambo hayo ataponyoka adhabu? Je, anaweza kuvunja agano na bado aponyoke?^d

16 ““Kwa hakika kama ni navyoishi,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, “atafia huko Babiloni, mahali ambapo anaishi mfalme* aliyemweka^e kuwa mfalme, ambaye alikidharau kiapo chake na ambaye alilivunja agano lake.^e 17 Na lile jeshi kubwa na wanajeshi wengi wa Farao hawatamsaidia kamwe vitani,^f wakati boma la kuzingira litakapojengwa na kuta za kuzingira zitakapojengwa ili kuangamiza uhai wa* watu wengi. 18 Amedharau kiapo na kuvunja agano. Hata ingawa alitoa ahadi,* amefanya mambo hayo yote, naye hataponyoka.”

19 “Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Kwa hakika kama ninavyoishi, nitamletea juu ya kichwa chake madhara ya kudharau kiapo changu^g na kuvunja agano langu. 20 Nitautandaza wavu wangu juu yake, naye atakamatwa katika wavu wangu wa kuwindia.^h Nitamletea Babiloni na kumhukumu huko kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu alionitendea.ⁱ 21 Wakimbizi wote kati ya wanajeshi wake watatawa kwa upanga, na wale wanaobaki watatawanyika

17:16 *Yaani, Nebukadneza. ^eYaani, Sedekia. 17:17 *Au “nafsi za.” 17:18 *Tnn., “aliutoa mkono wake.”

kila upande.*^a Ndipo mtakapolazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.”^b

22 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Nitachukua chipukizi kutoka katika kilele cha mwerezi mku-bwa^c na kulipanda, kutoka juu ya matawi yake nitakata chipukizi changa,^d nami mwenyewe nitalipanda juu ya mlima mrefu na ulio juu sana.”^e

23 Nitalipanda juu ya mlima mrefu wa Israeli; na matawi yake yatakua, nalo litazaa matunda na kuwa mwerezi mku-bwa. Na ndege wa kila aina wataishi chini yake na kuka kwenye kivuli cha majani yake. **24** Na miti yote ya shambani italazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimeushusha ule mti mrefu na kuukweza ule mti mfupi;^f nimeukausha ule mti mbichi na kuufanya mti uliokauka usitawi.^g Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema nami nimefanya hivyo.”^h

18 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Methali hii mnayoisema katika nchi ya Israeli inamaanisha nini, ‘Akina baba wamekula zabibu chachu, lakini meno ya wana ndiyo yanayotitwa ukakasi?’^h

3 “Kwa hakika kama ninavyoishi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘hamtaendelea kuutaja msemu huo katika Israeli. **4** Tazama! Nafsi zote—ni zangu.* Kama nafsi ya baba ilivyo yangu ndivyo ilivyo nafsi ya

17:21 *Tnn., “kwa kila upepo.” 18:4 *Au “Uhai wote—ni wangu.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 17

a Eze 12:14

b Eze 6:13

c Isa 11:1
Yer 23:5

d Isa 53:2

e Zb 2:6

f Isa 9:6
Eze 21:26, 27
Da 4:17
Amo 9:11

g Isa 2:7, 8
Lu 1:52

SURA YA 18

h Yer 31:29, 30

Safu ya 2

a Kum 12:2
Yer 3:6

b Law 20:10

c Law 18:19
Law 20:18

d Met 14:21

e Kum 24:12, 13

f Law 6:2, 4

g Kum 15:11

h Isa 58:6, 7
Yak 2:15, 16

i Kut 22:25
Zb 15:5
Lu 6:34, 35

j Law 19:35

k Law 19:15
Law 25:14
Kum 1:16

l Law 18:5

m Law 19:13

n Mwa 9:6
Kut 21:12

o Kum 15:7, 8

mwana—ni zangu. Nafsi* inayotenda dhambi ndiyo itakayokufa.”[#]

5 “Ikiwa mtu ni mwadilifu na anatenda haki na uadilifu, **6** naye hali dhabihu zinazotolewa kwa sanamu kwenye milima;^a hazitumaini sanamu zinazochukiza* za watu wa nyumba ya Israeli; hamnajisi mke wa jirani yake^b au kulala na mwanamke aliye katika hedihi;^c **7** hamtesi mtu yeyote,^d bali hurudisha rehani aliyopewa na mtu mwenye deni lake;^e hamnyang’anyi yeyote,^f bali humpa mwenye njaa chakula chake^g na kumfunika kwa vazi aliye uchi;^h **8** hatozai faida wala kutoza riba,ⁱ lakini anajizuia asitende isivyo haki;^j anatekeleza haki ya kweli kati ya mtu na mwenzake;^k **9** naye anaendelea kutembea katika amri zangu na kushika sheria zangu* ili atende kwa uaminifu. Mtu huyo ni mwadilifu na kwa hakika ataendelea kuishi,^l asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

10 “Lakini ikiwa yeye ni baba ya mwana ambaye ni mnyang’anyi^m au muuaji*ⁿ au anayefanya lolote kati ya mambo haya mengine **11** (ingawa baba yake hajafanya lolote kati ya mambo hayo)—anakula dhabihu zilizotolewa kwa sanamu kwenye milima, anamnajisi mke wa jirani yake, **12** anawatesa wenyewe uhitaji na maskini,^o anawanyang’anya watu vitu vyao,

18:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au “Mtu anayetenda dhambi ndiye atakayekufa.” 18:6 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau. 18:9 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.” 18:10 *Tnn., “mtu anayemwaga damu.”

harudishi kitu kilichowekwa rehani; anatumaini sanamu zinazochukiza,^a anajihusisha na mazoea yanayochukiza,^b **13** ametoza riba na kutoza faida—basi mwana huyo hataendelea kuishi. Kwa sababu ya mambo hayo yote yanayochukiza aliyofanya, kwa haki-ka atauawa. Damu yake mwenyewe itakuwa juu yake.

14 “Lakini ikiwa baba ana mwana anayeona dhambi zote anazofanya baba yake, na ingawa anazona, hafanyi mambo kama hayo, **15** hali dhabihu zilizotolewa kwa sanamu kwenye milima; hazitumaini sanamu zinazochukiza za watu wa nyumba ya Israeli; hamnajisi mke wa jirani yake; **16** hamteshi mtu yeyote; habaki na kitu kilichowekwa rehani; hamnyang’anyi mtu kitu chochote; chakula chake mwenyewe anampa mwenye njaa na kumfunika kwa vazi aliye uchi; **17** anaepuka kuwakandamiza maskini; hatenzi riba wala kutoza faida; naye anafuata sheria zangu;* ametembea kati-ka amri zangu. Mtu huyo hatakuwa kwa sababu ya kosa la baba yake. Kwa hakika ataendelea kuishi. **18** Lakini kwa kuwa baba yake alifanya ulaghai, akamnyang’anya ndugu yake, na kufanya mambo mabaya kati ya watu wake, atakufa kwa sababu ya kosa lake.

19 “Nanyi mtasema: “Kwa nini mwana hana hatia kwa sababu ya kosa la baba yake?” Kwa kuwa mwana ametenda mambo ya haki na ya uadilifu, amezishika amri zangu

18:17 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

SURA YA 18

a Law 26:30

b 2Fa 21:11

c Eze 22:12

Safu ya 2

a Kum 16:20
Ro 10:5b Kum 24:16
Yer 31:30
Eze 18:4c Isa 3:10, 11
Gal 6:7d Isa 55:7
Eze 3:21
Eze 33:12, 19
Mdo 3:19e 2Nya 33:12, 13
Zb 25:7
Isa 43:25

f Eze 33:16

g Omb 3:33
Eze 33:11
1Ti 2:3, 4
2Pe 3:9

h Mik 7:18

i Eze 33:12, 18
Ebr 10:38
2Yo 8j Met 21:16
Eze 3:20k Ayu 35:2
Met 19:3
Eze 33:17, 20

l Kum 32:4

m Isa 55:9
Yer 2:17

zote na kuzitenda, kwa hakika ataendelea kuishi.^a **20** Nafsi inayotenda dhambi ndiyo itakayokufa.^b *Mwana hatakuwa na hatia kwa sababu ya kosa la baba yake, na baba hatakuwa na hatia kwa sababu ya kosa la mwanawe. Mwadilifu atathawabishwa kwa sababu ya uadilifu wake mwenyewe, na mwovu ataadhibiwa kwa sababu ya uovu wake mwenyewe.^c

21 “Sasa mtu mwovu aki-ziacha dhambi zote alizofanya na kushika amri zangu na kutenda mambo ya haki na ya uadilifu, kwa hakika ataendelea kuishi. Hatakufa.^d **22** Hatahukumiwa kwa kosa lolote alilotenda.^e Ataendelea kuishi kwa kutenda uadilifu.^f

23 “Je, ninafurahia hata kidogo kifo cha mtu mwovu?^g asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Je, sipendelei kwamba aziache njia zake naye aendelee kuishi?’^h

24 “Lakini mtu mwadilifu akiacha uadilifu wake na kutenda kosa,* na kufanya mambo yote yanayochukiza wanayofanya waovu, je, ataiishi? Hakuna jambo lolote litakalokumbukwa kati ya matendo ya uadilifu aliyotenda.ⁱ Atakufa kwa sababu ya ukosefu wake wa uaminifu na dhambi aliyotenda.^j

25 “Lakini mtasema: “Njia ya Yehova si ya haki.”^k Tafadhali sikilizeni, enyi watu wa nyumba ya Israeli! Je, ni njia yangu isiyo ya haki?^l Je, si njia zenu ambazo si za haki?^m

18:20 *Au “Mtu anayetenda dhambi ndiye atakayekufa.” **18:22** *Tnn., “Kosa lolote alilotenda halitakumbukwa.” **18:24** *Au “kutenda jambo lisilo la haki.”

26 “Mtu mwadilifu akiuacha uadilifu wake na kutenda kosa, naye afe kwa sababu ya kosa hilo, atakufa kwa sababu ya kosa lake mwenyewe.

27 “Na mtu mwovu akiacha uovu ambao ametenda na kuanza kutenda mambo ya haki na ya uadilifu, atauhifadhi uhai wake* mwenyewe.^a

28 Akitambua na kuacha makosa yote ambayo ametenda, kwa hakika ataendelea kuishi. Hatakuufa.

29 “Lakini watu wa nyumba ya Israeli watasema: “Njia ya Yehova si ya haki.” Je, ni kweli kwamba ni njia zangu ambazo si za haki, enyi watu wa nyumba ya Israeli?^b Je, si njia zenu ambazo si za haki?”

30 “Kwa hiyo, nitamhukumu kila mmoja wenu kulingana na njia zake,^c enyi watu wa nyumba ya Israeli,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Acheni, naam, acheni kabisa makosa yenu yote, ili yasiwe kikwazo kinachowaletea hatia. **31** Jiondolee ni makosa yenu yote mliyofanya^d na mjipatie* moyo mpya na roho mpya,^e kwa nini mfe,^f enyi watu wa nyumba ya Israeli?”

32 “Mimi sifurahii kifo cha mtu yeyote,^g asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Kwa hiyo geukeni na kuishi.’”^h

19 “Nawe lazima uimbe wimbo wa huzuni* kuhusu wakuu wa Israeli, **2** useme,

‘Mama yako alikuwa nani?
Simba jike kati ya simba.

18:27 *Au “ataihifadhi nafsi yake.” Angalia Kamusi, uku. **2012. 18:31** *Tnn., “mjitengezee.” **19:1** *Au “wimbo wa maombolezo.”

SURA YA 18

a Isa 55:7
1Ti 4:16

b Mwa 18:25
Zb 145:17
Isa 40:14

c Ayu 34:11
Ro 2:6

d Zb 34:14
Isa 1:16

e Zb 51:10
Yer 32:39
Eze 11:19
Efe 4:23, 24

f Kum 30:15
Met 8:36
Mdo 13:46

g Yer 29:11
Omb 3:33
Eze 33:11
Lu 15:10
2Pe 3:9

h Kum 30:16

Safu ya 2

SURA YA 19

a 2Nya 36:1

b 2Fa 23:31-34
2Nya 36:4
Yer 22:11, 12

c Yer 22:17

d Met 28:15

Alilala kati ya wanasimba wenye nguvu* naye akawalea watoto wake.

3 Alimlea mmoja wa watoto wake, akawa mwanasimba mwenye nguvu.^a

Naye akajifunza jinsi ya kurarua mawindo, Akamnyafua hata mwanaadamu.

4 Mataifa yalisikia kumhusu na wakamkamata katika shimo lao,

Nao wakamleta kwa kulabu nchini Misri.^b

5 Mama huyo alisubiri na hatimaye akaona hakuna tumaini kwamba atarudi.

Basi akamchukua mwingine kati ya watoto wake na kumtuma akiwa wanasimba mwenye nguvu.

6 Yeye pia alitembea huku na huku kati ya simba, naye akawa mwanasimba mwenye nguvu.

Akajifunza jinsi ya kurarua mawindo, na hata akawanyafua wanaadamu.^c

7 Akazungukazunguka katika minara yao yenye ngome na kuyaharibu majiji yao,

Hivi kwamba nchi iliyo ukiwa ikajaa sauti ya mngurumo wake.^d

8 Mataifa ya wilaya jirani yalikuja dhidi yake ili kuitandaza wavu wao juu yake,

Naye akanaswa katika shimo lao.

9 Wakamweka katika kizimba kwa kulabu na ku-

19:2 *Au “wanasimba wenye manyoya marefu shingoni.”

mpeleka kwa mfalme wa Babiloni.

Wakamfunga huko ili sauti yake isisikike tena kwenye milima ya Israeli.

- 10** Mama yako alikuwa kama mzabibu^a katika damu yako, * uliopandwa kando ya maji.

Ukazaa matunda na kujaa matawi kwa sababu ya maji mengi.

- 11** Nao ukatokeza matawi yenye nguvu, * yanayofaa kuwa fimbo za ufalme za watawala.

Ukakua, ukawa mrefu kulioko miti mingine,

Nao ukaonekana kwa sababu ya urefu wake na wingi wa majani yake.

- 12** Lakini aling'olewa kwa ghadhabu^b na kutupwa chini ardhini,

Na upepo wa mashariki ukayakausha matunda yake.

Matawi yake yenye nguvu yalikatwa yakakauka,^c na moto ukayateketeza.^d

- 13** Sasa amepandwa nyikani, Katika nchi isiyo na maji na yenye kiu.^e

- 14** Moto ukaenea kutoka kwenye matawi yake* na kuteketeza machipukizi yake na matunda yake, Na hakuna tawi lenye nguvu lililobaki, hakuna fimbo ya mfalme ya kutawala.^f

“Huo ni wimbo wa huzuni, nao utatumiwa kama wimbo wa huzuni.”

19:10 *Au labda, “kama mzabibu katika shamba lako la mizabibu.” **19:11** *Au “fimbo zenye nguvu.” **19:14** *Au “fimbo zake.”

SURA YA 19

a Zb 80:8
Isa 5:7

b Isa 5:5
Eze 15:6

c 2Fa 23:34
2Fa 24:6
2Fa 25:5-7

d Kum 32:22
Eze 15:4

e Kum 28:48
Yer 17:5, 6
Yer 52:27

f Eze 17:16, 18

Safu ya 2

SURA YA 20

a Isa 1:12, 15
Eze 14:3

b Eze 16:51
Eze 22:2
Lu 11:47

c Kum 7:6

d Kut 4:31
Kut 6:7, 8

e Kut 3:8

20 Katika mwaka wa saba, mwezi wa tano, siku ya kumi ya mwezi huo, baadhi ya wazee wa Israeli walikuja na kuketi mbele yangu ili kuniomba ushauri kutoka kwa Yehova. **2** Ndipo neno la Yehova likanijia likisema: **3** “Mwana wa binadamu, zungumza na wazee wa Israeli uwaambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Je, mnakuja kuniomba ushauri? ‘Kwa hakika kama ninavyoishi, sitawajibu,’^a asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

4 “Je, uko tayari kuwahukumu?* Mwana wa binadamu je, uko tayari kuwahukumu? Wajulishe mambo yanayochukiza ambayo mababu zao walifanya.^b **5** Waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Siku nilipoi-chagua Israeli,^c pia niliupia* uzao wa[#] nyumba ya Yakobo, na kujijulisha kwao nchini Misri.^d Naam, niliwaapia na kusema, ‘Mimi ni Yehova Mungu wenu.’ **6** Siku hiyo niliapa kwamba nitawatoa nchini Misri na kuwapeleka katika nchi niliyokuwa nimeichunguza* kwa ajili yao, nchi inayotiririka maziwa na asali.^e Nchi hiyo ilikuwa nzuri sana kuliko[#] nchi zote. **7** Kisha nika waambia, ‘Lazima kila mmoja wenu atupe vitu vinavyochukiza vilivyo mbele ya macho yake; msijitie unajisi kwa sanamu zinazochukiza* za

20:4 *Au “kuwatangazia hukumu.”

20:5 *Tnn., “niliinua mkono wangu kwa.” #Tnn., “mbegu ya.”

20:6 *Au “nimeipeleleza.” #Au “pambo la.”

20:7 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

Misri.^a Mimi ni Yehova Mungu wenu.^b

8 ““Lakini wakianasi nao hawakutaka kunisikiliza. Hawakuvitupa vitu vinavyochukiza vilivyokuwa mbele yao, nao walikataa kuziacha sanamu zinazochukiza za Misri.^c Basi nikaahidi kuwamwagia ghadhabu yangu na kuwaletea hasira yangu yote nchini Misri. **9** Lakini nilichukua hatua kwa ajili ya jina langu ili lisichafuliwe mbele ya mataifa ambamo waliishi.^d Niliijulisha kwao* mbele ya mataifa hayo nilipowatoa* nchini Misri.^e **10** Kwa hiyo nikawatoa nchini Misri na kuwaongoza kuingia nyikani.^f

11 ““Kisha nikawapa amri zangu na kuwajulisha sheria zangu,^g ili mtu anayezifuata apate uzima kupitia hizo.^h **12** Pia nikawapa sabato zangu,ⁱ ziwe ishara kati yangu nao,^j ili wajue kwamba mimi, Yehova, ndiye ninayewatakasa.

13 ““Lakini watu wa nyumba ya Israeli waliniasi nyikani.^k Hawakutembea katika amri zangu, nao wakakataa sheria zangu,* ambazo mtu akizifuata, atapata uzima kupitia hizo. Walizitia unajisi kabisa sabato zangu. Basi nikaahidi kuwamwagia ghadhabu yangu nyikani ili niwaangamize kabisa.^l **14** Nilichukua hatua kwa ajili ya jina langu mwenyewe ili lisichafuliwe mbele ya mataifa, walioona nikiwatoa* huko.^m **15** Pia nikawaapia wakiwa nyikani

20:9, 14, 22 *Yaani, Waisraeli. 20:11, 13, 21 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

SURA YA 20

a Law 18:3
Kum 29:16, 17
Yos 24:14

b Law 20:7

c Kut 32:4

d Hes 14:13-16
Kum 9:27, 28
1Sa 12:22

e Kut 32:11, 12
Yos 2:9, 10
Yos 9:3, 9
1Sa 4:7, 8

f Kut 13:17, 18
Kut 15:22

g Kum 4:8

h Kum 8:3
Kum 30:16

i Kut 20:8-10
Law 23:3, 24
Law 25:4, 11

j Kut 31:13
Kut 35:2

k Kut 32:8
Hes 14:22, 23

l Hes 14:11, 12

m Yos 7:9
Eze 36:22

Safu ya 2

a Hes 14:30
Zb 95:11
Zb 106:26, 27

b Hes 13:26, 27

c Kut 32:1, 4
Hes 25:1, 2
Mdo 7:42

d Hes 14:33

e Zb 78:8

f Kum 4:1

g Yer 17:22

h Kut 31:13

i Hes 25:1
Kum 9:23

j Isa 63:10

k Zb 78:38

l Zb 25:11
Zb 79:9
Yer 14:7
Da 9:19

kwamba sitawapeleka katika nchi niliyowapa^a—nchi inayotiririka maziwa na asali,^b nchi nzuri sana kuliko* nchi zote— **16** kwa sababu walizikataa sheria zangu* na hawakutembea katika amri zangu, nao wakazitia unajisi sabato zangu, kwa maana mioyo yao ilikuwa ikifuata sanamu zao zinazochukiza.^c

17 ““Lakini niliwasikitikia,* nami sikuwahaaribu; si kuwaangamiza kabisa nyikani. **18** Niliwaambia wana wao nyikani,^d “Msitembee katika masharti ya mababu zenu^e wala kushika hukumu zao wala kujichafua kwa sanamu zao zinazochukiza. **19** Mimi ni Yehova Mungu wenu. Tembeeni katika amri zangu, na kuzishika sheria zangu,* na kuzifuata.^f **20** Nanyi zitakaseni sabato zangu,^g nazo zitakuwa ishara kati yangu nanyi ili mjue kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu.^h

21 ““Lakini wana hao wa-kaanza kuniasi.ⁱ Hawakutembea katika amri zangu, nao hawakushika wala kufuata sheria zangu,* ambazo mtu akizifuata, atapata uzima kupitia hizo. Walizitia unajisi sabato zangu. Basi nikaahidi kuwamwagia ghadhabu yangu, na kuwaletea hasira yangu yote nyikani.^j **22** Lakini nilijizuia^k na kuchukua hatua kwa ajili ya jina langu mwenyewe,^l ili lisichafuliwe mbele ya mataifa, walioona nikiwatoa* huko. **23** Pia, niliwa-

20:15 *Au “pambo la.” 20:16 *Tnn., “waliyakataa maamuzi yangu ya hukumu.” 20:17 *Tnn., “jicho langu liliwasikitikia.” 20:19 *Tnn., “kuyashika maamuzi yangu ya hukumu.”

pia nyikani kwamba nitawatawanya miongoni mwa mataifa na kuwatawanya katika nchi mbalimbali,^a **24** kwa sababu hawakufuata sheria zangu* na walikataa amri zangu,^b walizitia unajisi sabato zangu, nao wakafuata[#] sanamu zinazochukiza za mababu zao.^c **25** Pia, niliwaruhusu wafuate masharti ambayo hayakuwa mazuri na sheria* ambazo hazingewasaidia kupata uzima.^d **26** Nami nikawaacha watiwe unajisi kwa dhabihu zao wenyewe—walipomteketeka* motoni kila mzaliwa wa kwanza^e—ili kuwafanya wawe ukawa, ili wajue kwamba mimi ni Yehova.”

27 “Basi zungumza na watu wa nyumba ya Israeli, ewe mwana wa binadamu, nawe uwaambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Kwa njia hii pia, mababu zenu walinikufuru kwa kunitendea kwa ukosefu wa uaminifu. **28** Niliwaleta katika nchi niliyoapa kwamba ningewapatia.^f Walipoona vilima vyote virefu na miti yenye majani mengi,^g walianza kutoa dhabihu zao na matoleo yao yanayochukiza. Walitoa harufu inayopendeza* ya dhabihu zao na kumwaga matoleo yao ya vinywaji hapo. **29** Basi nikawauliza, ‘Mahali hapa pa juu mnapoenda panamaanisha nini? (Bado panaitwa Mahali pa Juu mpaka leo hii.)’”^h

30 “Sasa waambie watu wa nyumba ya Israeli, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ana-

20:24 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.” #Tnn., “macho yao yakafuata.”

20:25 *Tnn., “maamuzi ya hukumu.”

20:26 *Tnn., “walipompitisha.” 20:28 *Au “inayotuliza.”

SURA YA 20

a Law 26:33
Zb 106:26, 27

b Law 26:15, 16

c Yer 2:7

d Zb 81:12

e Law 18:21
Yer 7:31

f Yos 23:5

g Kum 12:2

h Eze 16:24, 25

Safu ya 2

a Amu 2:19
2Nya 21:13
Yer 13:26, 27

b Kum 18:10, 12
Zb 106:36-38
Yer 7:31

c Isa 1:15

d Zek 7:13

e Yer 44:17

f Yer 21:5
Eze 8:18

g Isa 27:13
Eze 34:16

h Yer 2:9

sema hivi: “Je, mnajichafua kama mababu zenu walivyo-fanya kwa kuzifuata sanamu zao zinazochukiza ili kufanya nazo ukahaba wa kiroho?^a **31** Na je, bado mnajichafua mpaka leo hii kwa kuzitolea dhabihu sanamu zenu zote zinazochukiza, mkiwateketeka* motoni wana wenu?^b Je, wakati huohuo ninapaswa kujibu maombi yenu, enyi watu wa nyumba ya Israeli?”^c

“Kwa hakika kama ninavyoishi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘Sitajibu maombi yenu.^d **32** Na jambo mnalofikiria mnaposema, “Na tuwe kama mataifa, kama familia za nchi nyngine, wanaoabudu* miti na mawe,”^e jambo hilo halitatimia kamwe.”

33 “Kwa hakika kama ninavyoishi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘Nitawatawala nikiwa mfalme kwa mkono wenye nguvu, kwa mkono ulionyooshwa, na kwa ghadhabu kali.^f **34** Kwa mkono wenye nguvu, kwa mkono ulionyooshwa, na kwa ghadhabu kali nitawatoa kati ya mataifa na kuwakusanya pamoja kutoa katika nchi ambazo mmetawanywa.^g **35** Nitawapeleka katika nyika ya mataifa na huko nitawahukumu uso kwa uso.^h

36 “Kama nilivyowahukumu mababu zenu katika nyika ya nchi ya Misri, ndivyo nitakavyowahukumu ninyi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **37** ‘Nitawafanya mpite chini ya fimbo ya

20:31 *Tnn., “mkiwapitisha.” 20:32 *Au “wanaohudumia; wanaotumikia.”

mchungaji^a na kuwaleta chini ya wajibu wa* agano. **38** Lakini nitawaondoa waasi kati yenu na wale wanaonitendea dhambi.^b Kwa maana nitawatoa katika nchi wanayokaa wakiwa wageni, lakini hawataingia katika nchi ya Israeli;^c nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^d

39 "Nanyi, enyi watu wa nyumba ya Israeli, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Kila mmoja wenu na aende kuziabudu sanamu zake zinazochukiza.^d Lakini baadaye ikiwa hamtanisikiliza, hamtaweza tena kulichafua jina langu takatifu kwa dhahibu zenu na kwa sanamu zenu zinazochukiza.'^e

40 "Kwa maana katika mlima wangu mtakatifu, kwenye mlima mrefu wa Israeli,^f asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'ndiko watu wote wa nyumba ya Israeli, wote, watanitumikia nchini.^g Nitafurahisha nao huko, nami nitadai mnipe michango yenu na matunda ya kwanza ya matoleo yenu, vitu vyenu vyote vitakatifu.^h **41** Kwa sababu ya harufu inayopendeza,* nitafurahishwa nanyi nitakapowatoa kati ya mataifa na kuwakusanya pamoja kutoka katika nchi ambazo mmetawanywa;ⁱ nami nitatakaswa kati yenu mbele ya macho ya mataifa.^j

42 "Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova^k nitakapowapeleka katika nchi ya Israeli,^l katika nchi ambayo niliapa kwamba nitawapa mababu zenu. **43** Na huko mtakumbuka mwenendo wenu na

20:37 *Tnn., "katika kifungo cha."
20:41 *Au "inayotuliza."

SURA YA 20

a Law 27:32
Eze 34:17

b Eze 34:20, 21

c Eze 13:9

d Amu 10:14
Zb 81:12

e Isa 1:13
Eze 23:39

f Isa 2:2, 3
Isa 66:20

g Isa 56:7
Zek 8:22

h Mal 3:4

i Isa 11:11
Yer 23:3

j Isa 5:16
Eze 38:23

k Eze 36:23

l Eze 11:17

Safu ya 2

a Law 26:40
Eze 6:9
Eze 16:61

b Yer 31:18

c Zb 79:9
Eze 36:22, 23

d Kum 32:22
Yer 21:14

e Isa 66:24

f 2Nya 7:20
Omb 2:17

matendo yenu yote ambayo mlijichafua kupitia hayo,^a nanyi mtajichukia* kwa sababu ya mambo yote mabaya mliyotenda.^b **44** Ndipo mtakapolazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakaposhughulika nanyi kwa ajili ya jina langu,^c si kulingana na mwendo wenu mwovu au kulingana na matendo yenu yaliyopotoa, enyi watu wa nyumba ya Israeli,^d asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

45 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **46** "Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako upande wa eneo la kusini na utangaze kuelekea kusini, na utabirie msitu wa uwanja wa kusini. **47** Uambie msitu wa kusini, 'Sikia neno la Yehova. Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: "Ninawasha moto dhidi yako,^d nao utateketeza kila mti mbiichi na kila mti uliokauka ndani yako. Moto huo nao awaka hautazimwa,^e nao utachoma kila uso, kuanzia kusini mpaka kaskazini. **48** Na kila mwili utaona* kwamba Mimi mwenyewe, Yehova, nimeuwasha moto, ili usizimwe."^f

49 Nami nikasema: "Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Wanasema kunihusu, 'Je, hazungumzi kwa vitendawili?'"*

21 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** "Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako Yerusalemu, na utoe tangazo dhidi ya mahali patakatifu, na utabiri dhi-

20:43 *Tnn., "mtazichukia nyuso zenu."

20:48 *Au "watu wote wataona."

20:49 *Au "methali?"

di ya nchi ya Israeli. **3** Iambie nchi ya Israeli, 'Yehova anasema hivi: "Niko dhidi yako, nami nitauchomoa upanga wangu kutoka katika ala yake^a na kumkatilia mbali mwadilifu na mwovu kutoka kati yako. **4** Kwa kuwa nitamkatilia mbali kutoka kati yako mwadilifu na mwovu, upanga wangu utachomolewa kutoka katika ala yake dhidi ya wote wenye mwili,* kutoka kusini mpaka kaskazini. **5** Watu wote watalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimeuchomoa upanga wangu kutoka katika ala yake. Hautarudi tena kawe."'^b

6 "Nawe, mwana wa binadamu, lia kwa maumivu huku ukitetemeka,* naam, lia kwa uchungu mbele yao.^c **7** Na wakikuuliza, 'Kwa nini unalia kwa maumivu?' utasema, 'Kwa sababu ya habari fulani.' Kwa maana hakika itakuja, na kila moyo utayeyuka kwa woga na kila mkono utalegea na kila roho itahuzunika na kila goti litadondosha maji.*^d 'Tazama! Hakika itakuja—itatokea,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

8 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **9** "Mwana wa binadamu, tabiri, 'Yehova anasema hivi: "Sema, 'Upanga! Upanga^e umenolewa, nao umesuguliwa. **10** Umenolewa kwa ajili ya uchinjaji mkubwa; umesuguliwa ili uwakewake kama radi.'"^f

"Je, hatupaswi kushangilia?"

21:4 *Au "watu wote." 21:6 *Tnn., "kiuno chako kikitetemeka." 21:7 *Yaani, watajikojolea kwa sababu ya woga.

SURA YA 21

a Law 26:33

b Yer 23:20

c Isa 22:4
Yer 4:19
Eze 9:8

d Eze 7:15-17

e Isa 66:16
Yer 12:12
Amo 9:4

Safu ya 2

a Mwa 49:10
2Sa 7:12, 14

b Yer 25:9
Yer 51:20

c Eze 9:8
Mik 1:8

d Eze 19:1

e Yer 6:27

f 2Fa 25:7
Eze 19:14
Eze 21:26

g 2Fa 25:1, 2

h Eze 21:7

i Isa 1:24
Eze 5:13
Eze 16:42

"Je, utakataa* fimbo ya ufalme ya mwana wangu mwenyewe,^a kama unavyokataa kila mti?

11 "Umetolewa ili usuguliwe na kushikwa mkononi. Upanga huo umenolewa na kusuguliwa, ili utiwe mkononi mwa muuaji.^b

12 "Mwana wa binadamu, lia kwa sauti na uomboleze,^c kwa maana upanga umekuja dhidi ya watu wangu; uko dhidi ya wakuu wote wa Israeli.^d Na upanga huo utawaanngamiza pamoja na watu wangu. Kwa hiyo piga paja lako kwa huzuni. **13** Kwa maana uchunguzi umefanywa,^e na itakuwaje ikiwa upanga utaikataa fimbo ya ufalme? Haitaendelea* kuwapo,^f asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

14 "Nawe, mwana wa binadamu, tabiri na upige makofi na kusema mara tatu, 'Upanga! Ni upanga wa wale waliouawa, upanga wa uchinjaji mkubwa, unaowazunguka.^g

15 Mioyo yao itayeyuka kwa woga^h na wengi wataanguka katika malango ya jiji lao; nitawachinja kwa upanga. Naam, unawakawaka kama radi na umesuguliwa ili kuchinja! **16** Kata kwa makali upande wa kulia! Geukia upande wa kushoto! Nenda popote ambapo makali yako yanaelekezwa! **17** Nami pia nitapiga makofi na kuiridhisha ghadhabu yangu.ⁱ Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema."

18 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **19** "Nawe, mwana wa binadamu, chora

21:10 *Yaani, upanga wa Yehova. 21:13 *Au "Fimbo ya ufalme haitaendelea."

njia mbili ambazo upanga wa mfalme wa Babiloni utapitia. Zote mbili zitaanzia nchi ileile, na ishara iwekwe* mahali ambapo barabara inatengana ili kuingia katika yale majiji mawili. **20** Unapaswa kuchora njia moja ili upanga ushambulie jiji la Raba^a la Waamoni, na njia nyingine ili ushambulie jiji la Yerusalemu^b lenye ngome, nchini Yuda. **21** Kwa maana mfalme wa Babiloni amesimama ili kufanya uaguzi* kwenye njia panda, mahali ambapo zile barabara mbili zinatengana. Anaitikisa mishale. Anaomba ushauri kutoka kwa sanamu[#] zake; anachunguza ini. **22** Uaguzi* ulio katika mkono wake wa kulia umeelekezwa Yerusalemu, ili kuweka mitambo ya kubomolea, ili kutoa agizo la kuchinja, ili kupiga kelele za vita, kuweka kwenye malango mitambo ya kubomolea, kujenga boma la kuzingira, kujenga ukuta wa kuzingira.^c **23** Lakini utaonekana kama uaguzi* wa uwongo machoni pa wale[#] waliowaapia.^d Lakini anakumbuka hatia yao naye atawakamata.^e

24 "Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Mmfanya hatia yenu wenyewe ikumbukwe kwa kuyafunua makosa yenu na kufanya dhambi zenu zionekane katika matendo yenu yote. Kwa kuwa sasa mmekumbukwa, mtachukuliwa kwa nguvu.*'

21:19 *Tnn., "mkono uwekwe." 21:21, 23, 29 *Au "ubashiri." 21:21[#]Tnn., "terafimu." 21:22 *Au "Ubashiri." 21:23[#]Yaani, wakaaji wa Yerusalemu. 21:24 *Tnn., "kwa mkono."

SURA YA 21

a Yer 49:2
Eze 25:5
Amo 1:14

b 2Sa 5:9
2Nya 26:9
2Nya 32:2, 5
2Nya 33:1, 14

c Yer 32:24
Yer 52:4

d 2Nya 36:11, 13
Eze 17:13

e 2Fa 25:6, 7

Safu ya 2

a 2Nya 36:11, 13
Yer 24:8
Yer 52:1, 2
Eze 17:19

b 2Fa 25:5-7
Yer 52:8, 11
Eze 12:12, 13

c Eze 21:13

d Zb 75:7
Da 4:17

e Da 4:37
Lu 21:24

f Mwa 49:10
Zb 89:3, 4
Zb 110:1
Isa 9:6
Isa 11:10
Lu 1:32, 33
Ufu 5:5

g Zb 2:6, 8
Da 7:13, 14
Lu 22:29

h Eze 25:5

i Yer 49:2, 3

25 "Lakini siku yako imefika, ewe uliyejeruhiwa vibaya, mkuu mwovu wa Israeli,^a wakati wa adhabu yako ya mwisho. **26** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Kiondoe kilemba, na ulivue taji.^b Hili halitabaki kama lili vyo.^c Mwinue aliye chini,^d na umshushe aliye juu.^e **27** Nitaliharibu, nitaliharibu, nitaliharibu. Nalo halitakuwa la mtu yeyote mpaka yule aliye na haki ya kisheria atakapokuja,^f nami nitampa yeye.'^g

28 "Nawe, mwana wa binadamu, tabiri, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi kuhusu Waamoni na kuhusu matusi yao.' Sema, 'Upanga! Upanga umechomolewa kwa ajili ya kuchinja; umesuguliwa ili kunyafua na kuwakawaka kama radi. **29** Licha ya maono ya uwongo na uaguzi* wa uwongo kuwahusu ninyi, mtarundikwa juu ya waliouawa,[#] watu waovu ambao siku yao imefika, wakati wa adhabu yao ya mwisho. **30** Urudishe upanga katika ala yake. Nitakuhukumia mahali ulipoumbwa, katika nchi uliyojaliwa. **31** Nitakumwaga ghadhabu yangu. Nitakupulizia moto wa hasira yangu, nami nitakutia mikononi mwa watu wakatili, mafundi wa maangamizi.^h **32** Utakuwa kuni kwa ajili ya moto;ⁱ damu yako mwenyewe itamwagwa nchini, nawe hutakumbukwa tena, kwa maana mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.'"

22 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** "Nawe, mwana wa binadamu, je, uko tayari kulita-

21:29 *Tnn., "juu ya shingo za waliouawa."

ngazia hukumu* jiji lenye hatia ya damu^a na kulijulisha mambo yake yote yanayochukiza?^b **3** Nawe utasema, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: "Ewe jiji linalomwaga damu^c ndani yake, ambalo wakati wake unakuja,^d linalotengeneza sanamu zinazochukiza* ili kujichafua,^e **4** umwagaji wako wa damu umekufanya uwe na hatia,^f na sanamu zako zinazochukiza zimekufanya usiwe safi.^g Umeharakisha mwisho wa siku zako, na mwisho wa miaka yako umefika. Ndiyo sababu nitakufanya uwe kitu cha kushutumiwa na mataifa na kitu cha kudhihakiwa na nchi zote.^h **5** Nchi zilizo karibu nawe na zile zilizo mbali nawe zitakudhihaki,ⁱ wewe ambaye jina lako si safi na ambaye umejaa msukosuko. **6** Tazama! Kila mkuu wa Israeli aliye miongoni mwako anatumia mamlaka yake kumwaga damu.^j **7** Ndani yako wanamdharau baba yao na mama yao.^k Wanampunja mkaaji mgeni, na kumtesa ya tima na mjane."^l

8 "Unapadharau mahali pangu patakatifu, nawe unazitia unajisi sabato zangu.^m **9** Ndani yako kuna wachongezi wanaokusudia kumwaga damu.ⁿ Ndani yako wanakula dhabihu milimani na kuendeleza mwenendo mchafu ndani yako.^o **10** Ndani yako wanakidharau kitanda cha baba yao,^p nao wanamnajisi mwanamke asiye safi aliye

22:2 *Tnn., "je, utalihukumu, je, utalihukumu." 22:3 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno "mavi," nalo hutumiwa kuonyesha dharau. 22:10 *Tnn., "wanaufunua uchi wa baba yao."

SURA YA 22

a 2Fa 21:16

Yer 2:34

Mt 23:37

b Eze 16:51

c Eze 24:6

d Eze 12:25

e 2Fa 21:11

f Mwa 9:6

g Law 26:30

Eze 23:37

h Kum 28:37

1Fa 9:7

Zb 80:6

Eze 23:32

Da 9:16

i Zb 79:4

j Isa 1:23

Mik 3:1-3

Sef 3:3

k Kum 27:16

l Kut 22:21, 22

Zb 82:3

Isa 1:17

m Law 19:30

n Kut 23:1

Law 19:16

o Yer 13:27

p Law 18:7

Law 20:11

Safu ya 2

a Law 18:19

Law 20:18

b Law 18:20

Law 20:10

Yer 5:8

c Law 18:15

d Law 20:17

e Kut 23:8

Kum 27:25

Isa 1:23

f Kum 23:19

g Kut 22:25

Law 6:4, 5

h Eze 21:7

i Kum 4:27

Kum 28:25

j Isa 1:25

Eze 23:27

k Eze 6:13

l Met 17:3

Yer 6:28-30

katika hedhi.^a **11** Ndani yako mwanamume mmoja anatenda kwa njia inayochukiza na mke wa jirani yake,^b mwingine anamnajisi binti mkwe wake mwenyewe kwa mwenendo mchafu,^c na mwingine anamnajisi dada yake, binti ya baba yake mwenyewe.^d **12** Ndani yako wanapokea rushwa ili kumwaga damu.^e Unakopesha kwa riba^f au kwa faida,^g nawe unachukua pesa kwa nguvu kutoka kwa majirani zako.^h Naam, umenisahau kabisa,ⁱ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

13 "Tazama! Ninapiga makofi kwa kuwa nimechukizwa na faida isiyo ya haki ambayo umepata na kwa sababu ya matendo yako ya kumwaga damu yaliyo ndani yako. **14** Je, ujasiri* wako utadumu na mikonu yako itaendelea kuwa imara katika siku nita-kapokuchukulia hatua?^h Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema, nami nitachukua hatua. **15** Nitakutawanya miongoni mwa mataifa na kukutawanya katika nchi hizo,ⁱ nami nitakomesha uchafu wako.^j **16** Nawe utadharauliwa na mataifa, na utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova."^k

17 Na neno la Yehova likinjia tena likisema: **18** "Mwana wa binadamu, watu wa nyumba ya Israeli wamekuwa kama takataka isiyo na thamani kwangu. Wote ni shaba na bati na chuma na risasi katika tanuru. Wamekuwa takataka ya fedha.^l

19 "Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema

22:12 *Au "kutoza riba ya juu sana." 22:14 *Tnn., "moyo."

hivi: 'Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa kama takataka isiyoy na thamani,^a ninawakusanya pamoja ndani ya Yerusalemu. **20** Kama watu wanavyokusanya fedha na shaba na chuma na risasi na bati katika tanuru ili kuyapulizia moto madini hayo na kuyayeyusha, ndivyo nitakavyowakusanya ninyi kwa hasira yangu na kwa ghadhabu yangu, nami nitawapuliza na kuwayeyusha.^b **21** Nitawakusanya na kuwapuliza kwa moto wa ghadhabu yangu,^c nanyi mtayeyushwa ndani yake.^d **22** Kama fedha inavyoyeyushwa katika tanuru, ndivyo mtakavyoyeyushwa ndani yake; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimewamwagia ghadhabu yangu.'"

23 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **24** "Mwana wa binadamu, iambie hivi nchi hiyo: 'Wewe ni nchi ambayo haitasafishwa au kunyeshewa mvua katika siku ya ghadhabu. **25** Ndani yake manabii wake wamepanga njama,^e kama simba anayenguruma akirarua mawindo.^f Wanawanyafua watu. Wanachukua hazina na vitu vyenye thamani. Wamewafanya wengi kuwa wajane ndani yake. **26** Makuhani wake wamevunjia sheria yangu,^g nao wanaendelea kupatia unajisi mahali pangu patakatifu.^h Hawatofautishi kati ya kitu katakatifu na cha kawaida,ⁱ hawawajulishi watu kisicho safi na kilicho safi,^j na wanakataa kushika sabato zangu, nami nimechafuliwa kati yao. **27** Wakuu wake walio kati yake ni kama mbwamwitu wanaoruarua mawindo; wanamwaga

SURA YA 22

a Zb 119:119
Met 25:4

b Eze 21:31

c Kum 4:24
Zb 21:9
Yer 21:12

d Zb 68:2

e Yer 5:31
Yer 6:13, 14

f Mik 3:5

g Yer 2:8
Omb 4:13
Mik 3:11h Law 20:3
Law 22:2

i Law 10:10

j Law 11:46, 47

Safu ya 2

a Mik 3:1-3
Sef 3:3b Isa 30:10
Yer 23:25
Omb 2:14
Eze 13:9, 10c Isa 1:23
Isa 3:14
Yer 21:12
Mik 2:2d Kut 32:11
Zb 106:23

SURA YA 23

e Yer 3:6, 7

f Law 17:7
Kum 29:16, 17
Yos 24:14
Eze 20:8

damu na kuua watu* ili wapate faida isiyoy ya haki.^a **28** Lakini manabii wake wamepiga lipu matendo yao kwa kutumia chokaa. Wanaona maono ya uwongo na kufanya uaguzi* wa uwongo,^b nao wanasesema: "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi," wakati ambapo Yehova mwenyewe hajasema. **29** Watu wa nchi wamewapunja watu na kuwanyang'anya vitu vyao,^c wamewatesa wenye uhitaji na maskini, nao wamempunja mkaaji mgeni na kumnyima haki.'

30 "'Nilikuwa nikitafuta kati yao mtu ambaye angeurekebisha ukuta wa mawe au asimame mbele yangu katika shimo ukutani kwa ajili ya nchi, ili nisiiangamize,^d lakini sikumpata yeyote. **31** Basi nitawamwagia ghadhabu yangu na kuwaangamiza kabisa kwa moto wa ghadhabu yangu. Nitawaletea madhara ya njia yao juu ya kichwa chao wenyewe,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

23 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** "Mwana wa binadamu, kulikuwa na wanawake wawili waliokuwa mabinti za mama mmoja.^e **3** Wakawa makahaba huko Misri;^f tangu ujana wao walifanya ukahaba. Huko matiti yao yalitomaswa, na vifua vyao vya ubikira vilipapaswa-papaswa. **4** Yule mkubwa alitwa Ohola,* na dada yake Oholiba.^g Wakawa wangu nao wakazaa wana na mabinti. Kuhusu ma-

22:27 *Au "nafsi." 22:28 *Au "ubashiri." 23:4 *Maana yake "Hema Lake." #Maana yake "Hema Langu Limo Ndani Yake."

jina yao, Ohola ni Samaria,^a na Oholibana ni Yerusalemu.

5 "Ohola akaanza kufanya ukahaba^b alipokuwa wangu. Aliwatamani kwa uchu wapenzi wake,^c majirani zake Waashuru.^d **6** Walikuwa magavana waliovaa mavazi ya bluu na watawala wasaidizi—wote walikuwa vijana wanaovutia waliopanda farasi wao. **7** Akaendelea kufanya ukahaba na wana wote bora wa Ashuru, naye akajichafua^e kwa sanamu zina-zochukiza* za wale aliowatamani kwa uchu. **8** Hakucha ukahaba aliofanya huko Misri, kwa maana walilala naye alipokuwa kijana, nao walipapasa-papasa kifua chake cha ubikira na kummwagia uchu wao.*^f **9** Basi nikamtia mikononi mwa wapenzi wake, wana wa Ashuru,^g ambao aliwatamani kwa uchu. **10** Waliufunua uchi^h wake na kuwakamata wanawe na mabinti zake,ⁱ naye wakamuua kwa upanga. Akawa na sifa mbaya kati ya wanawake, nao waka-tekeleza hukumu dhidi yake.

11 "Dada yake Oholibana alipoona jambo hilo, akawa na uchu mbaya zaidi, na ukahaba wake ulikuwa mbaya kuliko wa dada yake.^j **12** Aliwatamani kwa uchu majirani zake wana wa Ashuru,^k magavana na watawala wasaidizi waliovaa mavazi ya kifahari na waliopanda farasi—wote walikuwa vijana wanaovutia. **13** Alipojichafua, niliona kwamba wote wawili walikuwa wamefuata

23:7 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno "mavi," nalo hutumiwa kuonyesha dharau. 23:8 *Au "kufanya naye uasherati."

SURA YA 23

a 1Fa 16:23, 24

b 1Fa 14:16
1Fa 21:25, 26

c Ho 2:5

d 2Fa 15:19
2Fa 17:3
Ho 5:13
Ho 7:11

e Ho 5:3

f Kut 32:1, 4
1Fa 12:28, 29
2Fa 10:29g 2Fa 15:29
1Nya 5:26

h Ho 2:10

i 2Fa 17:6
2Fa 18:11j Yer 3:6-8
Eze 16:46, 47

k 2Fa 16:7

Safu ya 2

a 2Fa 17:19

b Eze 16:29

c Yer 3:2
Eze 16:36, 37d Zb 106:39, 40
Yer 6:8
Yer 12:8

e Eze 16:25

f Eze 20:7

g Yos 24:14

h Eze 23:3

njia ileile.^a **14** Lakini alizidisha matendo yake ya ukahaba. Aliwaona wanaume waliochongwa ukutani, sanamu za Wakaldayo zilizochongwa na kupakwa rangi nyekundu, **15** wakiwa wamevaa mishipi kiunoni, na vilemba vikubwa kwenye vichwa vyao, nao walikuwa na sura kama za mashujaa, wote walifanana na Wababiloni, waliozaliwa katika nchi ya Wakaldayo. **16** Akaanza kuwatamani kwa uchu mara tu alipowaona, naye akawatuma wajumbe kwao huko Ukaldayo.^b **17** Basi wana wa Babiloni wakaendelea kuja kwenye kitanda chake cha mapenzi, nao wakamchafua kwa uchu wao.* Baada ya kuchafuliwa nao, akawaacha akiwa amechukizwa.

18 "Alipoendelea kufanya ukahaba kwa ushupavu na kufunua uchi wake,^c nilimwacha nikiwa nimechukizwa, kama nilivyomwacha dada yake nikiwa nimechukizwa.^d **19** Naye akaendelea kuzidisha matendo yake ya ukahaba,^e akizikumbuka siku za ujana wake alipofanya ukahaba nchini Misri.^f **20** Aliwatamani kwa uchu kama masuria wa wanaume ambao kiungo chao cha kiume ni kama cha punda na ambao viungo vyao vya uzazi ni kama vya farasi. **21** Ulitamani mwendo wako mchafu uliokuwa nao ulipokuwa kijana kule Misri^g walipopapasa-papasa kifua chako, matiti ya ujana wako.^h

22 "Kwa hiyo, ewe Oholibana, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

23:17 *Au "kwa uasherati wao."

'Ninawachochea wale walio-kupenda^a ambao uliwaacha ukiwa umechukizwa, nami nitawaleta ili wakushambulie kutoka kila upande,^b 23 wana wa Babiloni^c na Wakkaldayo^d wote, wanaume wa Pekodi^e na Shoa na Koa, pamoja na wana wote wa Ashuru. Wote ni vijana wanaovutia, magavana na watawala wasaidizi, mashujaa waliochaguliwa moja kwa moja,* wote wakiwa wamepanda farasi. 24 Watakushambulia kwa magari ya vita na magurudumu yenye kelele pamoja na umati mkubwa wa wanajeshi, pamoja na ngao kubwa na ngao ndogo* na kofia. Watajipanga kukuzunguka, nami nitawapa mamlaka ya kuhukumu, nao lazima wakuhukumu wapendavyo.^f 25 Nitakumwagia ghadhabu yangu, nao watakutendea kwa hasira kali. Watakata pua yako na masikio yako, na watu wako waliobaki watauawa kwa upanga. Watawachukua wana na mabinti zako, na watu wako wanaobaki watateketewa kabisa kwa moto.^g 26 Watakuvua mavazi yako^h na kuchukua vito vyako* maridadi.ⁱ 27 Nitaukomesha mwenendo wako mchafu na ukahaba wako^j ulioanza nchini Misri.^k Utaacha kuwatazama, na hutaikumbuka Misri tena.'

28 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Niko karibu kukutia mikononi mwa wale unaowachukia, wale ulio-waacha ukiwa umechukizwa.'

23:23 *Tnn., "walioitwa." 23:24 *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale. 23:26 *Au "mapambo yako."

SURA YA 23

a Eze 16:37
Hab 1:6

b Yer 6:22
Yer 12:9

c Eze 21:19

d 2Fa 24:2

e Yer 50:21

f Yer 39:5

g Eze 15:7
Eze 20:47

h Yer 13:22
Ufu 17:16

i Isa 3:18-23
Yer 4:30
Eze 16:39

j Isa 27:9
Eze 16:41
Eze 22:15

k Eze 23:3

l Yer 21:7

Safu ya 2

a Kum 28:49, 51

b Eze 16:36, 37
Eze 16:39

c Yer 2:18

d Zb 106:35, 36
Eze 6:9
Eze 23:7

e Yer 3:8
Eze 16:46, 47

f 2Fa 21:13
Yer 25:15
Da 9:12

g Isa 51:17

h Kum 28:37
1Fa 9:7
Omb 2:15

i Zb 75:8

j 1Fa 14:9
Ne 9:26
Isa 17:10
Yer 2:32
Yer 13:25

29 Watakutendea kwa chuki na kuchukua kila kitu ulichofanyia kazi kwa jasho^a nao watakuacha ukiwa uchi, bila chochote. Uchi unaoaibisha wa uasherati wako na mwendo wako mchafu na ukahaba wako utafunuliwa.^b 30 Utatendewa mambo hayo kwa sababu uliyafuata mbio mataifa kama kahaba,^c kwa sababu ulijichafua kwa sanamu zao zinazochukiza.^d 31 Umeifuata njia ileile alioifuata dada yako,^e nami nitakiweka kikombe chake mkononi mwako.^f

32 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

'Utakunywa kikombe kipa-na na chenyewe kina cha dada yako,^g

Nawe utakuwa kitu cha kuchekwa na kudhihakiwa, na kikombe hicho kina mambo hayo kwa wingi.^h

33 Utalemewa na* ulevi na huzuni,

Kikombe cha hofu na ukiwa,

Kikombe cha dada yako, Samaria.

34 Utalazimika kukinywa na kukimaliza kabisaⁱ na kuviguguna vigae vyake Kisha utayang'oa matiti yako.

"Kwa maana mimi mwenyewe nimesema," asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.'

35 "Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Kwa kuwa umenisahau nawe umenipuuza kabisa,*^j utapata madhara ya mwenye-

23:33 *Au "Utajawa na." 23:35 *Tnn., "umenitupa nyuma ya mgongo wako."

ndo wako mchafu na matendo yako ya ukahaba.”

36 Kisha Yehova akania- mbia: “Mwana wa binadamu, je, utatangaza hukumu dhidi ya Ohola na Oholiba^a na ku- waonyesha waziwazi mazoea yao yanayochukiza? **37** Wamefanya uzinzi,^{*b} na mikono yao ina damu. Hawajafanya uzinzi tu na sanamu zao zinazochukiza, bali pia wame- wateketeza[#] motoni wana wao walionizalia, kama chakula cha sanamu zao.^c **38** Isit- she, hili ndilo wamenifanyia: Walipatia unajisi mahali pa- ngu patakatifu siku hiyo, nao wakazitia unajisi sabato za- ngu. **39** Baada ya kuwachi- nja wana wao kama dhabihu kwa sanamu zao zinazochu- kiza,^d walikuja mahali pangu patakatifu ili kupatia unajisi^e siku hiyohiyo. Hivyo ndivyo walivyofanya ndani ya nyumba yangu mwenyewe. **40** Hata walimtuma mjumbe ili awaite wanaume waje ku- toka mbali.^f Walipokuwa wa- kija, ulioga na kujipaka rangi machoni na kujipamba kwa mapambo.^g **41** Nawe uka- keti kwenye kochi la kifahari^h ambalo mbele yake kuna meza iliyoandaliwa,ⁱ na juu yake uli- weka uvumba wangu^j na ma- futa yangu.^k **42** Sauti ya umati wa watu waliostarehe ilisikika huko, na miongoni mwao kulikuwa na walevi wa- liioletwa kutoka nyikani. Wa- liwavisha wanawake bangili kwenye mikono na mataji ma- ridadi kwenye vichwa vyao.

43 “Ndipo nikasema ku- mhusu yule aliyechakazwa na uzinzi: ‘Sasa ataendelea kufa-

23:37 *Yaani, uzinzi wa kiroho. #Tnn., “wamewapitisha.”

SURA YA 23

a Eze 23:4

b Ho 1:2
Yak 4:4c Law 18:21
2Fa 17:17, 18
Eze 16:36

d Yer 7:31

e Law 20:3

f Isa 57:9

g Yer 4:30

h Isa 57:7

i Isa 65:11

j Eze 8:10, 11

k Eze 16:17, 18

Safu ya 2

a Law 20:10

b Mwa 9:6
Eze 16:38c 2Fa 24:3, 4
Zb 106:38
Eze 23:37d Yer 15:4
Yer 25:9
Eze 16:40

e Law 20:2

f 2Nya 36:17

g 2Fa 25:9, 10
Yer 39:8

h 2Pe 2:6

i Eze 6:13

SURA YA 24

j 2Fa 25:1
Yer 39:1
Yer 52:4

nya ukahaba wake.’ **44** Basi wakaendelea kuingia kwake, kama mtu anavyoenda kwa kahaba. Hivyo ndivyo wali- vyoenda kwa Ohola na kwa Oholiba, wanawake wenye mwenendo mchafu. **45** La- kini watu waadilifu watamhu- kumu kwa hukumu ambayo uzinzi^a na umwagaji wa damu unastahili;^b kwa maana wao ni wanawake wazinzi na mikono yao ina damu.^c

46 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ana- sema hivi: ‘Jeshi litaletwa li- washambulie na kuwafanya kuwa kitu cha kutisha na kitu cha kuporwa.^d **47** Jeshi hilo litawapiga mawe^e na kuwaka- takata kwa panga zao. Wata- waua wana wao na mabinti wao^f na kuziteketeza nyumba zao kwa moto.^g **48** Nitako- mesha mwenendo wako mcha- fu nchini, na wanawake wote watajifunza somo nao hawa- taiga mwenendo wenu mcha- fu.^h **49** Watawaletea madha- ra ya mwenendo wenu mchafu na ya dhambi zenu kuhusiana na sanamu zenu zinazochuki- za; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Bwana Mwe- nye Enzi Kuu Yehova.”ⁱ

24 Neno la Yehova likani- jia tena katika mwaka wa tisa, mwezi wa kumi, siku ya kumi ya mwezi huo, likise- ma: **2** “Mwana wa binadamu, andika tarehe hii,^{*} siku hii- hii ya leo. Mfalme wa Babilo- ni ameanza kulishambulia Ye- rusalemu siku hiihii ya leo.^j **3** Na useme methali^{*} kuhusu nyumba ya uasi, sema hivi ku- wahuu:

24:2 *Tnn., “jina la siku.” 24:3 *Au “istiari.”

“Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Weka motoni chungu cha kupikia; * kiweke motoni na utie maji ndani yake.^a

4 Weka vipande vya nyama ndani yake,^b kila kipande kizuri,

Paja na bega; kijaze kwa mifupa bora zaidi.

5 Chukua kondoo bora zaidi katika kundi,^c na urundi-ke kuni chini ya chungu kuzunguka pande zote.

Chemsha vipande hivyo, na upike mifupa iliyo ndani yake.”

6 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

‘Ole wake jiji la umwagaji wa damu,^d chungu cha kupikia chenye kutu, ambacho kutu yake hai-jaondolewa!

Toeni nyama ndani yake, kipande kwa kipande;^e msizipigie kura.

7 Kwa maana damu yake imo ndani yake;^f aliimwaga juu ya mwamba ulio wazi.

Hakuimwaga ardhini, ili kuifunika kwa mavumbi.^g

8 Ili kuchochea ghadhabu ya kulipiza kisasi, Nimeiweka damu yake juu ya mwamba ulio wazi, unaong’aa

Ili isifunikwe.^h

9 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

‘Ole wake jiji linalomwaga damu!

24:3 *Au “chungu cha kupikia chenye mdomo mpana.”

SURA YA 24

a Eze 11:3

b Eze 11:7

c Yer 39:6

d 2Fa 21:16
Mik 7:2
Mt 23:35

e Eze 11:7, 9

f Yer 2:34

g Law 17:13
Kum 12:16

h 2Fa 24:3, 4

i Mt 23:37

Safu ya 2

a Yer 21:10
Yer 32:29
Eze 22:15

b Yer 5:3
Yer 6:29

c 2Nya 36:14
Eze 22:9

d Eze 5:12, 13
Eze 8:18

e Yer 13:14
Eze 5:11

f Eze 24:18, 21

Nitarundika rundo kubwa la kuni.

10 Rundika kuni na uwashe moto,

Chemsha nyama kabisa, umwage mchuzi mzito, na uiache mifupa iungue.

11 Kiweke chungu kisicho na kitu kwenye makaa ili kiwe moto

Ili shaba yake iwe moto kabisa.

Uchafu wake utayeyuka ndani yake,^a na kutu yake itateketezwa.

12 Ni jambo linalokatisha tamaa na kuchosha, Kwa maana kutu yake nyingi haitatoka.^b

Kitupeni motoni pamoja na kutu yake!’

13 “‘Uchafu wako ulisababishwa na mwenendo wako mchafu.^c Nilijaribu kukusafisha lakini hungeweza kuwa safi kutokana na uchafu wako. Hutakuwa safi mpaka ghadhabu yangu dhidi yako itakapotulia.^d **14** Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema. Itatendeka. Nitatenda bila kujizuia, bila huruma, bila kughairi.^e Watakuhukumu kulingana na njia zako na matendo yako,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

15 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **16** “Mwana wa binadamu, kwa pigo moja niko karibu kumwondoa mpenzi wako kutoka kwako.^f Hupaswi kuomboleza; * wala hupaswi kulia wala kutokwa na machozi. **17** Lia kimyakimya kwa maumivu, wala usifanye desturi za kuwaomboleza

24:16 *Au “kukipigapiga kifua chako.”

waliokufa.^a Jifunge kilemba chako,^b na uvae viatu vyako.^c Hupaswi kufunika masharubu yako,^{*d} na usile mkate ulioletewa na watu wengine.”^{##e}

18 Nami nikazungumza na watu asubuhi, na mke wangu akafa jioni. Basi asubuhi nikafanya kama nilivyoamriwa.

19 Watu walikuwa wakiniuliza: “Je, hutatambia jinsi mambo haya unayofanya yanavyotuhusu?” **20** Nikawajibu: “Neno la Yehova limenijia likisema, **21** ‘Waambie watu wa nyumba ya Israeli, “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Niko karibu kupatia unajisi mahali pangu patakatifu,^f chanzo cha fahari yenu kubwa, kitu mnachokipenda sana na tamaa ya moyo wenu. * Wana na mabinti wenu mliowaacha watauawa kwa upanga.^g **22** Nanyi mtalazimika kufanya kama nilivyofanya. Hamtafunika masharubu yenu, nanyi hamtakula mkate mliioletewa na watu wengine.^h **23** Vilemba vyenu vitakuwa kwenye vichwa vyenu na viatu vyenu kwenye miguu yenu. Hamtaomboleza wala kulia. Badala yake mtaoza katika makosa yenu,ⁱ na kila mmoja wenu atamlilia mwenzake kwa maumivu. **24** Ezekieli amekuwa ishara kwenu.^j Mtatenda kama alivyotenda. Jambo hilo litakapotukia, mtalazimika kujua kwamba mimi ndiye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.””

25 “Nawe, mwana wa binadamu, siku nitakapoondoa **24:17** *Au “mdomo wako wa juu.” *Tnn., “mkate wa wanadamu.” **24:21** *Au “kitu ambacho nafsi yenu inakihurumia.”

SURA YA 24

a Yer 16:5

b Law 10:6

c 2Sa 15:30

d Mik 3:7

e Yer 16:7

f Zb 74:7
Zb 79:1
Yer 7:14
Omb 1:10
Omb 2:7
Eze 9:7g 2Nya 36:17
Yer 6:11

h Eze 24:17

i Law 26:39
Eze 33:10j Isa 8:18
Isa 20:3
Eze 4:3

Safu ya 2

a Kum 28:32
Yer 11:22

b Eze 33:21

c Eze 3:26
Eze 33:22

SURA YA 25

d Mwa 19:36, 38

e Yer 49:1
Amo 1:13
Sef 2:9f 2Sa 12:26
Eze 21:20

ngome yao kutoka kwao —kitu maridadi kinachowaletea shangwe, kitu wanachokipenda sana, tamaa ya moyo wao*—pamoja na wana wao na mabinti wao,^a **26** utajulishwa jambo hilo na yule aliyeponyoka.^b **27** Siku hiyo utafungua kinywa chako na kuzungumza na yule aliyeponyoka, nawe hutakuwa tena bubu.^c Utakuwa ishara kwao, nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

25 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako kwa Waamoni,^d na utabiri dhidi yao.^e **3** Unapaswa kusema hivi kuhusu Waamoni, ‘Sikieni neno la Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Kwa sababu ulisema ‘Aha!’ dhidi ya mahali pangu patakatifu wakati palipotwi unajisi, na dhidi ya nchi ya Israeli ilipofanywa ukiwa, na dhidi ya watu wa nyumba ya Yuda, walipopeleka uhamishoni, **4** kwa hiyo, ninakutia mikononi mwa Watu wa Mashariki uwe mali yao. Watapiga kambi zao* ndani yako na kusimamisha mahema yao kati yako. Watakula matunda yako, na kunywa maziwa yako. **5** Nitelifanya jiji la Raba^f liwe malisho ya ngamia, na nchi ya Waamoni iwe mahali pa kupumzika kwa ajili ya mifugo; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.””

6 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu ulipiga

24:25 *Au “nafsi zao.” **25:4** *Au “kambi zao zenye ukuta.”

makofi^a na kupiga miguu yako chini nawe ukashangilia kwa dharau kubwa dhidi ya nchi ya Israeli,^b **7** kwa hiyo nitauyoosha mkono wangu dhidi yako ili nikutie mikononi mwa mataifa uwe kitu cha kuporwa. Nitakukatilia mbali kutoka kati ya mataifa na kukuharibu kutoka katika nchi hizi.^c Nitakuangamiza, nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^d

8 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu watu wa Moabu^d na Seiri^e wamesema, “Tazama! Nyumba ya Yuda ni kama mataifa mengine yote,” **9** ninauacha wazi mpaka* wa Moabu kwenye majiji yake ya mpakani, uzuri wa^f nchi yake, Beth-yeshimothi, Baal-meoni, hadi Kiriathaimu.^f **10** Nitaitoa pamoja na Waamoni kuwa mali ya watu wa Mashariki,^g ili Waamoni wasikumbukwe kati ya mataifa.^h **11** Nami nitatekeleza hukumu katika Moabu,ⁱ nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’

12 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Nchi ya Edomu imelipiza kisasi dhidi ya nyumba ya Yuda nayo imepata hatia kubwa kwa kulipiza kisasi dhidi yake;’ **13** kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Pia nitauyoosha mkono wangu dhidi ya Edomu na kuwaangamiza wanadamu na wanyama waliomo, nami nitaifanya kuwa ukiwa.^k Kuanzia Temani mpaka Dedani, watauawa kwa upanga.^l **14** ‘Nitalipiza kisasi dhidi ya Edomu kwa mko-

25:9 *Au “mteremko.” #Au “pambo la.”

SURA YA 25

a Omb 2:15

b Sef 2:8

c Yer 49:2
Amo 1:14

d Isa 15:1
Yer 48:1
Amo 2:1

e Kum 2:4

f Hes 32:37, 38
Yos 13:15, 19

g Eze 25:4

h Eze 21:28, 32

i Yer 48:1

j 2Nya 28:17
Zb 137:7
Omb 4:22
Amo 1:11
Oba 10

k Mal 1:4

l Yer 49:7, 8

Safu ya 2

a Isa 11:14
Isa 63:1

b Nah 1:2

c 2Nya 28:18
Isa 9:11, 12
Isa 14:29
Yer 47:1
Yoe 3:4-6
Amo 1:6

d Yer 25:17, 20
Sef 2:4

e Sef 2:5

f Yer 47:4

SURA YA 26

g Yoe 3:4-6
Amo 1:9

h Omb 1:1

i Isa 23:11
Amo 1:10
Zek 9:4

no wa watu wangu Waisraeli.^a Watawaletea watu wa Edomu hasira yangu na ghadhabu yangu, ili wapatwe na kisasi changu mwenyewe,^b asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

15 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu ya chuki yao isiyoyana mwisho, Wafilisti wamejaribu kwa nia ovu* kulipiza kisasi na kuleta maangamizi.^c **16** Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Ninauyoosha mkono wangu dhidi ya Wafilisti,^d nami nitawakatilia mbali Wakerethi^e na kuwaangamiza wakaaji wanaobaki wa pwani ya bahari.^f **17** Nitatekeleza matendo makubwa ya kisasi dhidi yao kwa adhabu kali, nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapoleta kisasi changu dhidi yao.””

26 Katika mwaka wa 11, siku ya kwanza ya mwezi, neno la Yehova lilinjia likisema: **2** “Mwana wa binadamu, kwa sababu Tiro amesema kuhusu Yerusalemu,^g ‘Aha! Lango la mataifa limevunjwa!’^h Kila kitu kitakuja kwangu, nami nitakuwa tajiri kwa sababu ameangamizwa;’ **3** kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Niko dhidi yako, Ee Tiro, nami nitayainua mataifa mengi dhidi yako, kama vile bahari inavyoinua mawimbi yake. **4** Wataziharibu kuta za Tiro na kuibomoa minara yake,ⁱ nami nitakwangu udongo na kumfanya awe mwamba ulio wazi, unaoing’aa. **5** Atakuwa uwanja wa

25:15 *Au “kwa dharau iliyo katika nafsi yao.”

kukaushia nyavu za kukokotwa katikati ya bahari.’^a

“Kwa maana mimi mwenyewe nimesema,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘naye ataporwa na mataifa. **6** Na vijiji vyake* vilivyo mashambani vitachinjwa kwa upanga, na watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’

7 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Ninamleta Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni dhidi ya Tiro kutoka kaskazini;^b yeye ni mfalme wa wafalme,^c akiwa na farasi,^d magari ya vita,^e wapanda farasi, na jeshi lenye wanajeshi[#] wengi. **8** Ataviangamiza kwa upanga vijiji vyako vilivyo mashambani, naye atajenga ukuta wa kuzingira na kujenga dhidi yako boma la kuzingira na kuinua ngao kubwa dhidi yako. **9** Ataponda kuta zako kwa mtambo wake wa kubomolea,* na kubomoa minara yako kwa mashoka yake.[#] **10** Farasi wake watakuwa wengi sana hivi kwamba watakufunika kwa mavumbi, na sauti ya wapanda farasi, magurudumu, na magari ya vita itafanya kuta zako zitikisike anapoiingia kwenye malango yako, kama wanaume wanaovamia jiji lenye kuta zilizobomolewa. **11** Kwato za farasi wake zitakanyaga-kanyaga barabara zako zote;^f atawaua watu wako kwa upanga, na nguzo zako kubwa zitaporomoka ardhini. **12** Wataiba mali

26:6 *Tnn., “mabinti zake.” 26:7 *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili. [#]Tnn., “watu.” 26:9 *Au “mtambo wake wa kushambulia.” [#]Au “panga zake.”

SURA YA 26

a Eze 27:32

b Yer 25:9
Eze 29:18

c Da 2:37

d Hab 1:8

e Yer 4:13

f Isa 5:28
Hab 1:8

Safu ya 2

a Eze 27:32, 33
Eze 28:5, 18
Zek 9:3

b Isa 23:16

c Eze 26:4, 5

d Eze 27:28

e Eze 27:35
Eze 32:10

f Eze 27:32

g Amo 1:9, 10

h Eze 28:2

zako, watapora bidhaa zako,^a watabomoa kuta zako, na kubomoa nyumba zako nzuri; kisha watayatupa mawe yako na mbao zako na udongo wako katika maji.’

13 “Nitakomesha kelele za nyimbo zako, na sauti ya vinubi vyako haitasikika tena.^b

14 Nami nitakufanya uwe jiwe lililo wazi, linalong’aa, nawe utakuwa uwanja wa kukaushia nyavu za kukokotwa.^c Hutajengwa tena kamwe, kwa maana mimi mwenyewe, Yehova, nimesema,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

15 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anamwambia Tiro hivi: ‘Je, visiwa havitatetemeika vitakaposikia sauti ya kuanguka kwako, wanaokaribia kufa* watakapokuwa wakilia kwa maumivu makali, na uchinjaji utakapokuwa ukiendelea ndani yako?’^d **16** Wakuu wote wa bahari hakika watashuka kutoka kwenye viti vyao vya ufalme na kuvua kanzu zao* na mavazi yao yaliyotariziwa, nao wataanza[#] kutetemeka. Wataketi chini na kuendelea kutetemeka na kukuangalia kwa mshangao.^e **17** Nao watakuambia wimbo wa huzuni*^f na kukuambia:

“Jinsi ulivyoangamia,^g wewe uliyekuwa na wakaaji kutoka baharini, jiji lililosifiwa;

Wewe na wakaaji wako mlikuwa wenye nguvu baharini,^h

Ukieneza hofu kwa wakaaji wote wa dunia!

26:15 *Tnn., “waliouawa.” 26:16 *Au “majoho yasiyo na mikono.” [#]Tnn., “watavikwa.” 26:17 *Au “wimbo wa maombolezo.”

18 Visiwa vitatetemeka siku utakapoanguka, Visiwa vya bahari vitakuwa na wasiwasi utakapoondoka.”^a

19 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Nitakapokufanya ukiwa kama majiji yasiyokaliwa, nitakapokulemea kwa mawimbi makubwa nawe ufunikwe kwa maji mengi,^b **20** nitakushusha wewe pamoja na wale wanaoshuka shimoni,^{*} kwa watu wa zamani za kale; nitakufanya ukae mahali pa chini zaidi, kama mahali pa zamani palipoachwa ukiwa, pamoja na wale wanaoshuka shimoni,^c ili usikaliwe. Kisha nitaitukuza[#] nchi ya walio hai.

21 “Nitakuletea hofu ya ghafla, nawe hutakuwapo tena.^d Watakutafuta, lakini hutapatikana tena kamwe,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

27 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Nawe, mwana wa binadamu, mwimbie Tiro wimbo wa huzuni,^{*e} **3** nawe umwambie Tiro,

‘Wewe unayekaa katika malango ya bahari, Mfanyabiashara wa mataifa ya visiwa vingi, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Ee Tiro, wewe mwenyewe umesema, ‘Nina urembo mkamilifu.’”

4 Maeneo yako yamo katika ti ya bahari, Na wajenzi wako wameukamilisha urembo wako.

26:20 *Au “kaburini.” [#]Au “nitaipamba.” **27:2** *Au “wimbo wa maombolezo.”

SURA YA 26

a Isa 23:5

b Eze 27:34

c Eze 28:8

d Eze 27:36

SURA YA 27

e Eze 26:17

f Isa 23:9
Eze 28:2, 12

Safu ya 2

a Kum 3:8, 9
1Nya 5:23

b Mwa 10:2, 4

c Mwa 10:2, 4

d Mwa 10:15, 18

e 1Fa 9:27

f Yos 13:2, 5

g Eze 27:27

h Mwa 10:6
Yer 46:9

5 Walitengeneza mbao zako zote kutokana na mibero shi ya Seniri,^a

Nao waliuchukua mwerezi kutoka Lebanoni ili kukutengenezea mlingoti.

6 Walitengeneza makasia yako kutokana na mialoni ya Bashani,

Na omo yako ilitengenezwa kwa mvinje na kupambwa ndani kwa pembe za tembo kutoka visiwa vya Kitimu.^b

7 Kitani chenye rangi mbalimbali kutoka Misri ndicho kilichokuwa tanga lako,

Na sitaha yako ilifunikwa kwa nyuzi za bluu na sufu ya zambarau kutoka visiwa vya Elisha.^c

8 Wakaaji wa Sidoni na Arvadi^d walikuwa wapiga makasia wako.

Watu wako mwenyewe wenyewe ustadi, Ee Tiro, walikuwa mabaharia wako.^e

9 Wanaume wa Gebali^f wenyewe uzoefu^{*} na ustadi waliziba nyufa zako kwa kalafati.^g

Meli zote za baharini na wanamaji wake walikuwa kwako kubadilishana bidaha.

10 Wanaume wa Uajemi, Ludi, na Putu^h walikuwa katika jeshi lako, wanauume wako wa vita.

Walitundika ngao na kofia zao ndani yako, nao walikuletea fahari.

11 Wanaume wa Arvadi katika jeshi lako walisimama juu ya kuta zako pande zote,

27:9 *Tnn., “wanaume wazee.”

Na wanaume jasiri walilinda minara yako.

Walitundika ngao zao za mvingo kuzunguka kuta zako

Nao wakaukamilisha urembo wako.

12 ““Watu wa Tarshishi^a walifanya biashara nawe kwa sababu ya utajiri wako mwingi.^b Walibadilisha fedha, chuma, bati, na risasi kwa ajili ya bidhaa zako.^c **13** Watu wa Yavani, Tubali,^d na Mesheki^e walifanya nawe biashara, wakibadilisha watumwa^f na vitu vya shaba kwa ajili ya bidhaa zako. **14** Watu wa nyumba ya Togarma^g walibadilisha farasi na farasi wa vita na nyumbu kwa ajili ya bidhaa zako. **15** Watu wa Dedani^h walifanya nawe biashara; uliwaajiri wafanyabiashara kwenye visiwa vingi; walitoa mpenbe za temboⁱ na mbao za mpingo kama ushuru wako. **16** Watu wa Edomu walifanya biashara nawe kwa sababu ya wingi wa bidhaa zako. Walitoa feruzi, safu ya zambarau, vitambaa vyenye rangi mbalimbali vilivyotariziwa, vitambaa bora, marijani, na zabarijadi ili kubadilishana na bidhaa zako.

17 ““Watu wa Yuda na wanchi ya Israeli walifanya nawe biashara, wakitoa ngano ya Minithi,^j vyakula bora, asali,^k mafuta, na zeri^l ili kubadilishana na bidhaa zako.^m

18 ““Watu wa Damaskoⁿ walifanya nawe biashara kwa sababu ya wingi wa bidhaa zako na utajiri wako wote, wakibadilishana divai ya Helboni na safu ya Zahari.* **19** Watu wa

27:18 *Au “sufu ya rangi nyekundu na kijivu.”

SURA YA 27

a Mwa 10:2, 4
Yon 1:3

b 2Nya 9:21

c Yer 10:9

d Isa 66:19

e Mwa 10:2

f Yoe 3:6

g Mwa 10:2, 3
Eze 38:6

h Mwa 10:7

i 1Fa 10:22

j Amu 11:12, 33

k Mwa 43:11

l Yer 8:22

m 1Fa 5:9
Ezr 3:7
Mdo 12:20

n Isa 7:8

Safu ya 2

a Mwa 25:3

b Mwa 25:13

c 2Nya 17:11
Isa 60:7

d Mwa 10:7

e 1Fa 10:1, 2
Isa 60:6

f Mwa 11:31

g 2Fa 19:12
Amo 1:5

h Mwa 25:3
Ayu 6:19

i Mwa 10:22

j 1Fa 10:22
Isa 23:14

Vedani na Yavani kutoka Uzali walitoa chuma kilichofuliwa, kida,* na kane[#] ili kubadilishana na bidhaa zako. **20** Watu wa Dedani^a walifanya nawe biashara kwa kupa matandiko ya farasi.* **21** Uliwaajiri Waarabu na wakuu wote wa Kedari,^b walio kuwa wafanyabiashara wa wanakondoo na kondoo dume na mbuzi.^c **22** Wafanyabiashara wa Sheba na Raama^d walibadilishana nawe bidhaa; walitoa kila aina ya manukato bora, mawe yenye thamani, na dhahabu, ili kubadilishana na bidhaa zako.^e **23** Watu wa Harani,^f Kane, Edeni,^g wafanyabiashara wa Sheba,^h Asihuru,ⁱ na Kilmadi walibadilishana nawe bidhaa. **24** Katika soko lako walibadilishana nawe mavazi maridadi, majoho yaliyotengenezwa kwa kitambaa cha bluu na vitambaa vyenye rangi mbalimbali vilivyotariziwa, na mazulia ya rangi mbalimbali, yote yakiwa yamefungwa kabisa kwa kamba.

25 Meli za Tarshishi^j zilisafirisha bidhaa zako katika misafara,

Hivi kwamba ukajaa na kulemewa na mzigo* katikati ya bahari kuu.

26 Wapiga makasia wako wamekuleta katika bahari kuu;

Upepo wa mashariki umekuvunjavunja katikati ya bahari kuu.

27 Utajiri wako, bidhaa zako, mali zako,

27:19 *Mti wa jamii ya mdalasini. [#]Utete wenye harufu nzuri. **27:20** *Au “matandiko yaliyotengenezwa kwa vitambaa vilivyofumwa.” **27:25** *Au labda, “na utukufu.”

wanamaji wako, na mabaharia wako,

Wale wanaoziba nyufa zako kwa kalafati, wale wanaofanya biashara ya kubadilishana bidhaa zako,^a na wanaume wote wa vita^b

—Umati wote ulio* ndani yako—

Wote watazama katikati ya bahari kuu siku utakayoanguka.^c

28 Mabaharia wako watakapolia kwa sauti, maeneo ya pwani yatatetemeka.

29 Wapiga makasia wote, wanamaji, na mabaharia Watashuka kutoka kwenye meli zao na kusimama kwenye nchi kavu.

30 Watapaza sauti zao na kukulilia kwa uchungu^d Huku wakijirushia mavumbi vichwani na kugaa-gaa kwenye majivu.

31 Watajitia upara na kuvaa nguo za magunia; Watakulilia kwa uchungu* na kukuombolezea sana.

32 Katika maombolezo yao watakuambia wimbo wa huzuni na kukuombolezea wakisema:

‘Ni nani aliye kama Tiro, ambaye sasa amenyamazishwa katikati ya bahari?’^e

33 Bidhaa zako zilipofika kutoka kwenye bahari kuu, uliyashibisha mataifa mengi.^f

Utajiri wako mwingi na bidhaa zako ziliwatajirisha wafalme wa dunia.^g

34 Sasa umevunjwavunjwa

SURA YA 27

a Eze 27:8, 9

b Eze 27:10, 11

c Eze 26:14

d Isa 23:1
Eze 26:17

e Eze 26:5

f Eze 27:14, 16

g Zek 9:3

Safu ya 2

a Eze 26:19

b Eze 27:27

c Eze 26:15

d Eze 28:17

e Zb 37:10

SURA YA 28

f Eze 28:5

g Eze 27:4

h Da 2:48

i Zek 9:3

katika bahari kuu, katika vilindi vya bahari,^a

Na bidhaa zako zote na watu wako wamezama pamoja nawe.^b

35 Wakaaji wote wa visiwani watakutazama kwa mshangao,^c

Nao wafalme wao watatetemeka kwa hofu^d—nyuso zao zitakuwa na wasiwasi.

36 Wafanyabiashara miongoni mwa mataifa watapiga mluzi kwa sababu ya yale yatakayokupata.

Mwisho wako utafika ghafla nao utakuwa mbaya sana,

Nawe hutakuwapo tena kamwe.^{*****e}

28 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, mwambie kiongozi wa Tiro, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Kwa sababu moyo wako umekuwa na majivuno,^f unaendelea kusema, ‘Mimi ni mungu.

Ninaketi kwenye kiti cha ufalme cha mungu katikati ya bahari.’^g

Lakini wewe ni mwanadamu tu, wewe si mungu,

Ingawa moyoni mwako unahisi kwamba wewe ni mungu.

3 Tazama! Una hekima kuliko Danieli.^h

Hujafichwa siri yoyote.

4 Umejitatirisha kwa hekima yako na utambuzi wako,

Nawe unaendelea kukusanya dhahabu na fedha katika hazina zako.ⁱ

27:27 *Tnn., “Kutaniko lolote lililo.”
27:31 *Au “kwa uchungu wa nafsi.”

5 Ustadi wako katika biashara ulikuletea utajiri mwingi,^a

Nao moyo wako ukawa na majivuno kwa sababu ya utajiri wako.”

6 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Kwa sababu katika moyo wako unahisi wewe ni mungu,

7 Ninawaleta wageni waku-shambulie, walio wakati-li zaidi kati ya mataifa,^b Nao watachomoa panga zao na kuuharibu uzuri wa hekima yako

Na kuitia unajisi fahari yako yenye utukufu.^c

8 Watakushusha shimoni,* Nawe utakufa kifo cha kikatili katikati ya bahari kuu.^d

9 Je, bado utamwambia yule anayekuu, ‘Mimi ni mungu?’

Utakuwa mwanadamu tu, wala si mungu, mikononi mwa wale wanaokutia unajisi.”

10 “Kwa mkono wa wageni, utakufa kifo cha watu ambao hawajatahiriwa, Kwa maana mimi mwenyewe nimesema, ‘asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

11 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **12** “Mwana wa binadamu, mwimbie mfalme wa Tiro wimbo wa huzuni,* nawe umwambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

28:8 *Au “kaburini.” **28:12** *Au “wimbo wa maambolezo.”

SURA YA 28

a Isa 23:1, 3
Eze 27:12

b Eze 30:10, 11

c Isa 23:9

d Eze 27:26

Safu ya 2

a Eze 28:3

b Eze 27:3

c Eze 27:16

d Isa 14:13

e Yoe 3:4
Amo 1:9

f Ifa 10:11
2Nya 9:21
Eze 27:12

g Yoe 3:6

h Isa 23:9
Yer 25:17, 22
Yer 47:4
Yoe 3:8

“Ulikuwa mfano wa ukamilifu,*

Ulijaa hekima^a nawe ulikuwa na urembo mkamilifu.^b

13 Ulikuwa katika Edeni, bustani ya Mungu.

Ulipambwa kwa kila jiwe lenye thamani

—Zabarijadi, topazi, na yaspi; krisolito, shohamu, na yashefi; yakuti, feruzi,^c na zumaridi;

Na vifuko na vishikizi vyake vilikuwa vya dhahabu.

Vilitayarishwa siku uliyoumbwa.

14 Nilikuweka kuwa kerubi anayefunika aliyetiwa mafuta.

Ulikuwa kwenye mlima mtakatifu wa Mungu,^d nawe ulitembea-tembea kati ya mawe yenye moto.

15 Hukuwa na kosa katika njia zako tangu siku uliyoumbwa

Mpaka uovu* ulipopatika-na ndani yako.^e

16 Kwa sababu ya biashara zako nyingi,^f

Ulijaa ukatili, nawe ukainza kutenda dhambi.^g

Basi nitakufukuza kutoka kwenye mlima wa Mungu kama kitu kilicho najisi na kukuangamiza,^h

Mbali kutoka kwenye mawe ya moto, ewe kerubi unayefunika.

17 Moyo wako ulikuwa na

28:12 *Tnn., “Ulikuwa ukifunga kielelezo kwa muhuri.” **28:15** *Au “ukosefu wa uadilifu.”

majivuno kwa sababu ya urembo wako.^a

Uliipotosha hekima yako kwa sababu ya fahari yako yenye utukufu.^b

Nitakutupa chini duniani.^c

Nitakufanya uwe kitu cha kutazamwa na wafalme.

18 Kwa sababu ya hatia yako kubwa na ukosefu wako wa unyoofu katika biashara, umepatia unajisi mahali pako patakatifu.

Nitatokeza moto katikati yako, nao utakutekeza kabisa.^d

Nitakufanya uwe majivu juu ya dunia mbele ya wote wanaokutazama.

19 Wale wote waliokujua kati ya mataifa watakutazama kwa mshangao.^e

Mwisho wako utafika ghafla nao utakuwa mbaya sana,

Hutakuwapo tena kamwe.^{****f}

20 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **21** “Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako Sidoni,^g nawe utabiri dhidi yake. **22** Nawe utasema, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Niko dhidi yako, Ee Sidoni, nami nitakuzwa katikati yako;

Na watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapotekeleza hukumu dhidi yake na kutakaswa ndani yake.

23 Nitapeleka ugonjwa hatari humo na damu itatiririka kwenye barabara zake.

Walioouawa wataanguka katikati yake upanga uta-

SURA YA 28

a Eze 27:3

b Isa 14:14

c Isa 14:15

d Amo 1:9, 10

e Eze 27:35

f Eze 27:36

g Isa 23:4
Yer 25:17, 22
Eze 32:30

Safu ya 2

a Eze 26:6

b Hes 33:55
Yos 23:12, 13

c Kum 30:3
Isa 11:12
Yer 30:18
Ho 1:11

d Isa 5:16

e Yer 23:8

f Mwa 28:13

g Isa 32:18
Yer 23:6
Ho 2:18

h Isa 65:21, 22
Yer 31:5
Amo 9:14

i Yer 30:16

SURA YA 29

j Yer 25:17, 19
Yer 43:10, 11
Eze 31:2

k Yer 46:25
Eze 31:18

kapokuja kumshambulia kutoka kila upande;

Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^a

24 ““Na watu wa nyumba ya Israeli hawatazungukwa tena na michongoma inayodhuru na miiba mikali,^b wale wanaowadhahiaki; na watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

25 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Nitakapowakusanya tena watu wa nyumba ya Israeli kutoka miongoni mwa mataifa walikotawanywa,^c nitatakaswa kati yao machoni pa mataifa.^d Nao watakaa katika nchi yao^e niliyompa mtumishi wangu Yakobo.^f **26** Wataishi huko kwa usalama^g na watajenga nyumba na kupanda mashamba ya mizabibu^h na watakaa kwa usalama nitakapotekeleza hukumu dhidi ya wote wanaowazunguka ambao wanawadhahiaki;ⁱ nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao.”

29 Katika mwaka wa kumi, mwezi wa kumi, siku ya 12 ya mwezi huo, neno la Yehova lilinijia likisema: **2** “Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako kwa Farao mfalme wa Misri, na utabiri dhidi yake na dhidi ya nchi yote ya Misri.^j **3** Sema maneno haya: ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Niko dhidi yako, Farao mfalme wa Misri,^k

Mnyama mkubwa sana wa baharini anayelala kati

ya vijito vya mto wake Nile,*^a

Ambaye amesema, 'Mto wangu Nile ni wangu. Niliutengeneza kwa ajili yangu.'^b

- 4 Lakini nitatia kulabu katika mataya yako na kufanya samaki wa mto wako Nile washikamane na magamba yako.

Nitakutoa katika mto wako Nile pamoja na samaki wa mto wako Nile wanaoshikamana na magamba yako.

- 5 Nitakuacha jangwani, wewe na samaki wote wa mto wako Nile.

Utaanguka uwanjani, nawe hutakusanywa wala kuokotwa.^c

Nitakufanya uwe chakula cha wanyama wa mwituni wa dunia na ndege wa angani.^d

- 6 Ndipo wakaaji wote wa Misri watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova, Kwa sababu kwa watu wa nyumba ya Israeli walikuwa kama unyasi* tu, hawakuwategemeza.^e

- 7 Walipokushika mkono, uli-pondwa, Nawe ukafanya wavunjike bega.

Walipojitegemeza kwako, ulivunjika,

Nawe ukafanya miguu yao ipesuke."^f

8 "Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ana-

29:3 *Kuanzia mstari huu, neno "Nile" linarejelea mto huo na mifereji yake ya kumwagilia mimea maji. 29:6 *Tnn., "utete." 29:7 *Tnn., "viuno vyao vipepesuke."

SURA YA 29

a Eze 32:2

b Eze 29:9

c Yer 25:33

d Eze 32:4

e Isa 36:6
Yer 37:5-7
Eze 17:17

f Yer 17:5

Safu ya 2

a Yer 46:14
Eze 30:4
Eze 32:12

b Yer 43:11-13

c Eze 29:3

d Eze 30:12

e Yer 44:1

f Eze 30:6, 7

g Eze 31:12
Eze 32:13

h Yer 46:19

i Eze 30:23

j Yer 46:25, 26

k Mwa 10:13, 14
Eze 30:14

l Eze 30:13

m Eze 32:2

sema hivi: "Ninaleta upanga ukushambulie,^a nami nitamwangamiza mwanadamu na mnyama kutoka ndani yako. 9 Nchi ya Misri itakuwa ukiwa na mahali palipoharibiwa;^b nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova, kwa maana umesema,* 'Mto Nile ni wangu; mimi ndiye niliyetengeneza.'^c 10 Basi niko dhidi yako na dhidi ya mto wako Nile, nami nitaifanya nchi ya Misri iwe mahali palipoharibiwa na palipokauka, mahame na ukiwa,^d kutoka Migdoli^e hadi Siene^f hadi kwenye mpaka wa Ethiopia. 11 Hakuna mwanadamu wala mnyama wa kufugwa atakayepitia humo kwa miguu,^g nayo haitakaliwa kwa miaka 40. 12 Nitaifanya nchi ya Misri iwe nchi yenye ukiwa kuliko nchi zote, na majiji yake yatakuwa majiji yenye ukiwa kuliko majiji yote kwa miaka 40;^h nami nitawatawanya Wamisri miongoni mwa mataifa na kutawatawanya katika nchi mbalimbali."ⁱ

13 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: "Baada ya miaka 40 nitawakusanya Wamisri kutoka katika mataifa ambako walitawanywa;^j 14 Wamisri waliotekwa nitawarudisha katika nchi ya Pathrosi,^k katika nchi waliyozaliwa, na huko watakuwa ufalme duni. 15 Misri itakuwa chini kuliko zile falme nyingine nayo haitayatawala tena yale mataifa mengine,^l nitawafanya wawe wadogo sana hivi kwamba hawataweza kuyatiisha mataifa mengine."^m 16 Nchi ya Misri

29:9 *Tnn., "amesema."

haitakuwa tena tegemeo kwa watu wa nyumba ya Israeli,^a bali itawakumbusha tu kosa walilofanya kwa kutafuta msaada kutoka kwa Wamisri. Nao watalazimika kujua kwamba mimi ndiye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.””

17 Sasa katika mwaka wa 27, mwezi wa kwanza, siku ya kwanza ya mwezi huo, neno la Yehova lilinjia likisema: **18** “Mwana wa binadamu, Mfalme Nebukadneza*^b wa Babiloni aliamuru jeshi lake lifanye kazi kubwa ya kushambulia Tiro.^c Kila kichwa kilitiwa upara, na kila bega lilisuguliwa na kuchubuka ngozi. Lakini yeye na jeshi lake hawakupata malipo yoyote kwa ajili ya kazi kubwa aliyofanya ya kuishambulia Tiro.

19 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Ninampa Mfalme Nebukadneza* wa Babiloni nchi ya Misri,^d naye atabeba utajiri wake na kuchukua nyara kwa wingi na kuipora; na vitu hivyo vitakuwa malipo ya jeshi lake.’

20 “Kama malipo ya kazi kubwa aliyofanya ya kushambulia Tiro, nitampa nchi ya Misri kwa sababu walitenda kwa ajili yangu,^e asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

21 “Siku hiyo nitaichipusha pembe kwa ajili ya watu wa nyumba ya Israeli,^{*f} nami nitakupa[#] nafasi ya kuzungumza kati yao; nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

29:18, 19 *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili. **29:21** *Au “nitawapa nguvu watu wa nyumba ya Israeli.” #Yaani, Ezekieli.

SURA YA 29

a Isa 30:2
Isa 36:4, 6
Yer 2:18
Yer 37:5-7

b Yer 25:9
Yer 27:3, 6

c Eze 26:7

d Yer 43:10, 12

e Eze 30:9, 10

f 1Sa 2:10
Lu 1:69

Safu ya 2

SURA YA 30

a Oba 15

b Eze 32:7

c Zb 110:6

d Eze 32:11, 12

e Sef 2:12

f Nah 3:8, 9

g Eze 30:18

h Yer 44:1

i Eze 29:10

j Yer 46:19
Eze 29:12
Eze 32:18

30 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, tabiri, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

“Ombolezeni, ‘Ole, ile siku inakuja!’

3 Kwa maana siku hiyo iko karibu, naam, siku ya Yehova iko karibu.^a

Itakuwa siku ya mawingu,^b wakati uliowekwa wa mataifa.^c

4 Upanga utaishambulia Misri, na Ethiopia itakumbwa na hofu wakati waliouawa watakapoanguka huko Misri;

Utajiri wake umechukuliwa na misingi yake imebomolewa kabisa.^d

5 Ethiopia,^e Putu,^f Ludi na watu wote wa mataifa mbalimbali,^{*}

Na Kubu, pamoja na wana wa nchi ya agano,[#]

Wote watauawa kwa upanga.”

6 Yehova anasema hivi: ‘Wale wanaoiunga mko-misri wataangamia pia,

Na nguvu zake zenye kiburi zitashushwa.’^g

“Kuanzia Migdoli^h mpaka Sieneⁱ watauawa kwa upanga nchini,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **7** ‘Watafanywa kuwa nchi yenye ukiwa zaidi, na majiji yake yatakuwa majiji yaliyoharibiwa kabisa.^j

8 Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapowasha moto huko Misri na wote walioungana naye wa-

30:5 *Au “wote waliotoka katika mataifa mengine.” #Huenda inarejelea Waisraeli walioungana na Misri.

takapopondwa. **9** Siku hiyo nitawatuma wajumbe katika meli ili kuifanya Ethiopia inayojitumaini itetemeke; wata-shikwa na hofu katika siku hiyo inayokuja dhidi ya Misri, kwa maana hakika itakuja.’

10 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Nitauangamiza umati wa Misri kwa mkono wa Mfalme Nebukadreza* wa Babiloni.^a

11 Yeye na wanajeshi wake, taifa katili zaidi kati ya mataifa,^b wataletwa ili kuiangamiza nchi. Watachomoa panga zao na kuishambulia Misri na kuijaza nchi watu waliouawa.^c **12** Nitaigeuza mifereji ya Nile^d iwe nchi kavu na kuiuza nchi mikononi mwa watu waovu. Nitaifanya nchi na kila kitu kilichomo kiwe ukiwa kwa mkono wa wageni.^e Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.’

13 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Nitaziangamiza pia sanamu zinazochukiza* na kuharibu miungu ya ubatili ya Nofu.^f Hakutakuwa tena na mkuu^g anayetoka katika nchi ya Misri, nami nitaweka hofu katika nchi ya Misri.^g **14** Nitalifanya jiji la Pathrosi^h liwe ukiwa na kuwasha moto katika jiji la Soani na kutekeleza hukumu dhidi ya jiji la No.ⁱ **15** Nitalimwagia ghadhabu yangu jiji la Sini, ngome ya Misri, na kuwaangamiza

30:10 *Tnn., “Nebukadreza,” njia nyingine ya kuandika jina hili. **30:13** *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau. **30:13, 16** ^aAu “Memfisi.” **30:13** ^aAu “kiongozi.” **30:14** *Yaani, Thebesi.

SURA YA 30

a Eze 29:19
Eze 32:11

b Hab 1:6

c Eze 29:5

d Eze 29:3

e Eze 31:12

f Yer 43:12
Yer 46:14

g Yer 46:5

h Mwa 10:13, 14
Yer 44:1

i Yer 46:25

Safu ya 2

a Eze 30:8

b Yer 46:20
Eze 31:18

c Yer 46:19

d Yer 46:25
Eze 29:3

e 2Fa 24:7
Yer 46:2

f Yer 46:21

g Eze 29:12

h Yer 27:6

i Eze 32:11, 12

wakaaji wa jiji la No. **16** Nitawasha moto nchini Misri; na jiji la Sini litashikwa na hofu na jiji la No litapenywa kwa nguvu na Nofu^f litashambuliwa kweupe kabisa wakati wa mchana! **17** Wanau-me vijana wa Oni* na Pibese-thi watauawa kwa upanga, na majiji yatapelekwa utekwani. **18** Kule Tehafnehesi mchana utakuwa na giza nitakapovunja nira za Misri huko.^a Nguvu zake zenye kiburi zitakwisha,^b mawingu yatamfunika, na miji yake itapelekwa utekwani.^c **19** Nitatekeleza hukumu dhidi ya Misri, nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

20 Na katika mwaka wa 11, mwezi wa kwanza, siku ya saba ya mwezi huo, neno la Yehova lilinjia likisema: **21** “Mwana wa binadamu, nimevunja mkono wa mfalme Farao wa Misri; hautafungwa upone au kufungwa kwa kitamba uwe na nguvu za kushika upanga.”

22 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Niko dhidi ya mfalme Farao wa Misri,^d nami nitavunja mikonu yake, mkono wenye nguvu na ule uliovunjika,^e nami nitaufanya upanga uanguke kutoka mkononi mwake.^f **23** Kisha nitawatawanya Wamisri miongoni mwa mataifa na kuwatawanya katika nchi mbalimbali.^g **24** Nitaitia nguvu mikono ya* mfalme wa Babiloni^h na kuu-tia upanga wangu mkononi mwake,ⁱ nami nitavunja mikono ya Farao, naye atalia kwa sauti na kwa maumivu makali

30:17 *Yaani, Heliopolisi. **30:24** *Au “nitaongeza nguvu za.”

kama mtu anayekufa mbele yake.* **25** Nitaitia nguvu mikono ya mfalme wa Babiloni, lakini mikono ya Farao italegea; nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapoutia upanga wangu mkononi mwa mfalme wa Babiloni naye aunyooshe dhidi ya nchi ya Misri.^a **26** Nami nitawawanya Wamisri miongoni mwa mataifa na kuwatawanya katika nchi mbalimbali,^b nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

31 Katika mwaka wa 11, mwezi wa tatu, siku ya kwanza ya mwezi huo, neno la Yehova lilinjia likisema: **2** “Mwana wa binadamu, mwambie mfalme Farao wa Misri na umati wake,^c

‘Unafanana na nani katika ukuu wako?’

3 Kulikuwa na Mwashuru, mwerezi kule Lebanoni, Uliokuwa na matawi mardadi kama kichaka chenye kivuli, na uliokuwa mrefu,

Kilele chake kilikuwa mawinguni.

4 Maji yaliufanya uwe mkubwa, chemchemi zenye maji mengi ziliufanya uwe mrefu.

Vijito vilizunguka mahali ulipopandwa;

Mifereji yake iliinywesha maji miti yote ya shambani.

5 Ndiyo sababu ulikuwa mrefu kuliko miti mingine yote ya shambani.

Na vitawi vyake viliongezeka, na matawi yake yakuwa marefu

30:24 *Yaani, mbele ya mfalme wa Babiloni.

SURA YA 30

^a Eze 29:19, 20

^b Eze 29:12

SURA YA 31

^c Yer 46:2
Eze 29:2

Safu ya 2

^a Mwa 2:8
Eze 28:12, 13

Kwa sababu ya maji mengi ya vijito vyake.

6 Ndege wote wa angani walitengeneza viota kwenye vitawi vyake,

Wanyama wote wa mwituni walizaa chini ya matawi yake,

Na mataifa yote yenye watu wengi yaliishi chini ya kivuli chake.

7 Ukapendeza katika uzuri na urefu wa matawi yake,

Kwa maana mizizi yake ilipenya chini kwenye maji mengi.

8 Hakuna mwerezi mwingine katika bustani ya Mungu^a uliofanana nao.

Hakuna mberoshi uliokuwa na vitawi kama vyake,

Na hakuna mwaramoni uliokuwa na matawi yaliyofanana na yake.

Hakuna mti mwingine katika bustani ya Mungu uliokaribia uzuri wake.

9 Niliufanya upendeze, kwa majani mengi,

Na miti mingine yote ya Edeni, bustani ya Mungu wa kweli, ili uonea wivu.’

10 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa sababu ulikuwa* mrefu sana, ukainua kilele chake mawinguni, nao moyo wake ukawa na kiburi kwa sababu ya kimo chake, **11** nitaitia mikononi mwa mtawala mwenye nguvu wa mataifa.^b Hakika atauadhibu, nami nitaukataa kwa sababu ya uovu wake. **12** Na wageni, wakati zaidi kati ya mataifa, wa-

^b Eze 30:10, 11
Hab 1:6

31:10 *Tnn., “wewe ulikuwa.”

taukata, nao watauacha milimani, nayo majani yake yataanguka katika mabonde yote, na matawi yake yatavunjika na kusambaa katika vijito vyote vya nchi.^a Mataifa yote ya dunia yataondoka kwenye kivuli chake na kuuacha.

13 Ndege wote wa angani wataishi kwenye shina lake liloanguka, na wanyama wote wa mwituni kwenye matawi yake.^b **14** Itakuwa hivyo ili mti wowote ulio karibu na maji usiwe mrefu sana au usiue kilele chake mwinguni na kusiwe na mti ulionyeshwa maji mengi utakaofikia kimo chao. Kwa maana miti yote itatiwa mikononi mwa kifo, kwenye nchi iliyo chini, pamoja na wana wa binadamu, wanaoshuka shimoni.[#]

15 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: 'Siku utakaposhuka kuingia Kaburini* nitasababisha maombolezo. Kwa hiyo, nitayafunika maji yenye kina na kuvizua vijito vyake ili maji yake mengi yazuiwe. Nitatia giza Lebanoni kwa sababu yake, nayo miti yote ya shambani itanyauka. **16** Nitayafanya mataifa yatetemeke kwa sauti ya kuanguka kwake nitakapushusha Kaburini* pamoja na wote wanaoshuka shimoni,[#] na miti yote ya Edeni,^c miti iliyo bora na iliyo mizuri kabisa ya Lebanoni, miti yote iliyonyeshwa maji mengi, itafarijiwa katika nchi iliyo chini. **17** Wameshuka Kaburini* pamoja naye, kwa wale waliouawa kwa upanga,^d pamoja na wale waliomsaidia[#]

31:14, 16 ^aAu "kaburini." 31:15-17 ^aAu "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. 31:17 ^aTnn., "mkono wake."

SURA YA 31

a Eze 32:5, 6

b Eze 29:5
Eze 32:4

c Eze 31:9

d Eze 32:18, 20

Safu ya 2

a Eze 30:6
Eze 32:31b Eze 31:9
Eze 32:19

SURA YA 32

c Isa 51:9, 10
Eze 29:3

ambao waliishi katika kivuli chake kati ya mataifa.^a

18 "Ni mti gani katika Edeni uliofanana nawe kwa utukufu na ukuu?^b Lakini kwa hakika utashushwa pamoja na miti ya Edeni katika nchi iliyo chini. Utalala kati ya wale ambao hawajatahiriwa, pamoja na wale waliouawa kwa upanga. Itakuwa hivyo kwa Farao na umati wake wote,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

32 Na katika mwaka wa 12, mwezi wa 12, siku ya kwanza ya mwezi huo, neno la Yehova lilinjia tena likisema: **2** "Mwana wa binadamu, mwimbie wimbo wa huzuni* mfalme Farao wa Misri, nawe umwambie,

'Ulikuwa kama mwanasimba[#] mwenye nguvu wa mataifa,

Lakini umenyamazishwa.

Ulikuwa kama mnyama mkubwa sana wa baharini,^c ukitibua maji katika mito yako,

Ukivuruga maji kwa miguu yako na kuchafua mito.'^Δ

3 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

'Nitautumia umati wa mataifa mengi kutandaza wavu wangu juu yako, Nao watakukokota katika wavu wangu wa kukokotwa.

4 Nitakuacha nchini; Nitakutupa uwanjani. Nitawafanya ndege wote wa angani watue juu yako,

32:2 ^aAu "wimbo wa maombolezo." [#]Au "mwanasimba mwenye manyoya marefu shingoni." ^ΔTnn., "mito yao."

- Nami nitawashibisha wanyama wa mwituni wa dunia nzima kwa nyama yako.^a
- 5** Nitaitupa nyama yako juu ya milima
Na kuyajaza mabonde mabaki yako.^b
- 6** Nitailowesha nchi kwa damu yako inayobubujika, mpaka juu ya milima, Nayo itajaa kwenye vijito.*
- 7** 'Na utakapozimwa nitazifunika mbingu na kuzitia giza nyota zake.
Nitalifunika jua kwa mawingu,
Na mwezi hautatoa nuru yake.^c
- 8** Kwa sababu yako, nitaitia giza mianga yote inayong'aa mbinguni,
Nami nitaifunika nchi yako kwa giza,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.
- 9** 'Nitaitaabisha mioyo ya mataifa mengi nitakapowapeleka watu wako waliotekwa katika mataifa mengine,
Katika nchi ambazo huzijui.^d
- 10** Nitayafanya mataifa mengi yashikwe na hofu,
Na wafalme wao watatetemeka kwa woga kwa sababu yako nitakapoutikisa upanga wangu mbele yao.
Wataendelea kutetemeka, kila mmoja akihofia uhai wake,
Siku utakayoanguka.'
- 11** Kwa maana Bwana Mwe-

32:6 *Tnn., "Nawe utazijaza sakafu za vijito."

SURA YA 32

a Eze 29:5

b Eze 31:12

c Isa 13:1, 10

d Eze 29:12
Eze 30:26

Safu ya 2

a Yer 43:10, 11
Yer 46:25, 26
Eze 30:24b Eze 30:10, 11
Hab 1:6

c Eze 29:19

d Eze 30:12

e Eze 29:8, 11

f Zb 107:33, 34
Eze 29:12

g Eze 30:26

nye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

'Upanga wa mfalme wa Babiloni utakushambulia.^a

- 12** Nitaufanya umati wako uuawe kwa panga za mashujaa hodari,
Walio wakatili zaidi kati ya mataifa,^b
Watawashusha chini kiburi cha Misri, na umati wake wote utaangamizwa.^c

- 13** Nitaiangamiza mifugo yake yote kando ya maji yake mengi,^d

Na hakuna mguu wa mwanadamu au ukwato wa mnyama wa kufugwa utakaoyachafua tena.^e

- 14** 'Wakati huo nitayasafisha kabisa maji yao,
Nami nitafanya mito yao itiririke kama mafuta,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

- 15** 'Nitakapoifanya nchi ya Misri iwe mahame na ukiwa, nchi iliyoporwa vitu vyote vilivyoijaza,^f
Nitakapowaua wakaaji wote walio ndani yake,
Watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^g

- 16** Huu ni wimbo wa huzuni, na hakika watu watauimba;
Mabinti wa mataifa watauimba.

Wataiambia nchi ya Misri na umati wake wote,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

- 17** Kisha katika mwaka wa 12, siku ya 15 ya mwezi huo, neno la Yehova lilinjia likisema: **18** "Mwana wa binadamu, uombolezee umati wa Misri nawe umshushe kwenye nchi

iliyo chini, yeye na mabinti wa mataifa yenye nguvu, pamoja na wale wanaoshuka chini shimoni.*

19 “Unamzidi nani kwa urembo? Shuka chini, ulale na watu ambao hawajatahiriwa!”

20 “Wataanguka miongoni mwa wale waliouawa kwa upanga.^a Ametiwa mikononi mwa upanga; mkokote pamoja na umati wake wote.

21 “Kutoka kwenye vina vya Kaburi* mashujaa hodari zaidi watazungumza naye na wasaidizi wake. Hakika watashuka chini na kula kama watu ambao hawajatahiriwa, waliouawa kwa upanga. **22** Ashuru yuko huko pamoja na umati wake wote. Makaburi yao yamemzunguka, wote wameuawa kwa upanga.^b **23** Makaburi yake yamo katika vina vya shimo,* na umati wake umezunguka kaburi lake, wote wameuawa kwa upanga, kwa sababu walisababisha hofu katika nchi ya walio hai.

24 “Elamu^c yuko huko pamoja na umati wake wote kuzunguka kaburi lake, wote wakiwa wameuawa kwa upanga. Wameshuka chini bila kutahiriwa katika nchi iliyo chini, wale waliosababisha hofu katika nchi ya walio hai. Sasa watabeba aibu yao pamoja na wale wanaoshuka chini shimoni.* **25** Wamemtengenezea kitanda kati ya watu waliouawa, pamoja na umati wake wote kuzunguka makaburi yake. Wote hawajatahiriwa, na waliuawa kwa upanga,

32:18, 24, 25, 29 *Au “kaburini.”
32:21, 27 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 32:23 *Au “kaburi.”

SURA YA 32

a Eze 29:8

b Isa 37:36
Zek 10:11

c Mwa 10:22
Yer 49:34, 35

Safu ya 2

a Mwa 10:2
Eze 38:2

b Mwa 25:30
Isa 34:5
Eze 25:12, 13
Amo 1:11
Oba 1
Mal 1:4

c Yer 9:25, 26

d Mwa 10:15
Eze 28:21

kwa sababu walisababisha hofu katika nchi ya walio hai; nao watabeba aibu yao pamoja na wale wanaoshuka chini shimoni.* Amewekwa miongoni mwa wale waliouawa.

26 “Watu wa Mesheki na Tubali^a na umati wao* wote wako huko. Makaburi yao yamemzunguka. Wote hawajatahiriwa, wamechomwa kwa upanga, kwa sababu walisababisha hofu katika nchi ya walio hai. **27** Je, hawatalala pamoja na mashujaa hodari waliouawa ambao hawajatahiriwa, ambao walishuka Kaburini* wakiwa na silaha zao za vita? Nao wataweka panga zao chini ya vichwa vyao[#] na dhambi zao kwenye mifupa yao, kwa sababu mashujaa hawa hodari walisababisha hofu katika nchi ya walio hai. **28** Lakini wewe, utapondwa miongoni mwa watu ambao hawajatahiriwa, nawe utalala pamoja na wale waliouawa kwa upanga.

29 “Edomu^b yuko huko, wafalme wake na wakuu wake wote, ambao ingawa walikuwa hodari, walilazwa miongoni mwa wale waliouawa kwa upanga; wao pia watalala na watu ambao hawajatahiriwa^c na pamoja na wale wanaoshuka chini shimoni.*

30 “Wakuu* wote wa kasazini wako huko, pamoja na Wasidoni wote,^d ambao wameshuka kwa aibu pamoja na waliouawa, ingawa walisababisha hofu kwa nguvu zao. Watalala wakiwa hawajatahiriwa

32:26 *Tnn., “wake.” 32:27 [#]Huenda inarejelea mashujaa waliozikwa wakiwa na panga zao, kwa heshima ya kijeshi.
32:30 *Au “Viongozi.”

pamoja na wale waliouawa kwa upanga nao watabeba aibu yao pamoja na wale wa-naoshuka chini shimoni.*

31 “Farao atawaona kwa wote, naye atafarijiwa kwa sababu ya mambo yote yaliyou-pata umati wake;^a Farao na jeshi lake lote watauawa kwa upanga,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

32 “Kwa kuwa alisababisha hofu katika nchi ya walio hai, Farao na umati wake wote wat-alazwa ili wapumzike pamoja na watu ambao hawajatahiri-wa, pamoja na wale walioua-wa kwa upanga,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

33 Na neno la Yehova va likanijia likisema: **2** “Mwana wa binadamu, zungumza na wana wa watu wako,^b uwaambie,

“Ikiwa nitaleta upanga uishambulia nchi,^c na watu wote wa nchi hiyo wamchukue mtu fulani na kumfanya awe mlinzi wao, **3** naye aone upanga ukija kuishambulia nchi, kisha apige pembe na kuwanya watu,^d **4** ikiwa mtu atasi-kia sauti ya pembe lakini asitii onyo,^e nao upanga uje na kumuua,* damu yake itaku-wa juu ya kichwa chake mwenyewe.^f **5** Aliisikia sauti ya pembe, lakini hakutii onyo. Damu yake itakuwa juu yake mwenyewe. Kama angetii onyo, angeokoa uhai wake.*

6 “Lakini mlinzi akiuona upanga ukija naye asipige pembe^g na watu wasipate onyo nao upanga uje na kumuua mmoja wao, mtu huyo atakufa kwa sababu ya kosa lake mwe-

SURA YA 32
a Eze 31:16

SURA YA 33

b Eze 3:11

c Law 26:25
Eze 6:3
Eze 21:9

d Yer 4:5
Ho 8:1

e Yer 6:17
Zek 1:4

f Eze 3:19
Mdo 18:6

g Isa 56:10

Safu ya 2

a Eze 3:18

b Isa 21:8
Yer 1:17
Eze 3:17

c Isa 3:11
Eze 18:4

d Met 11:21

e Met 15:10

f Eze 3:19
Mdo 18:6

g Law 26:39
Isa 64:6
Eze 24:23

h Eze 37:11

i Eze 18:23
ITI 2:3, 4

j Isa 31:6
Lu 15:10

k Zb 130:7, 8

l Isa 55:7
Yer 3:22
Yer 25:5
Mdo 3:19

m Eze 18:31
2Pe 3:9

n Eze 3:20
Eze 18:24

o 1Fa 8:48, 50
Eze 18:21

nyewe, lakini nitaidai damu yake kutoka kwa mlinzi.**^a

7 “Na wewe, mwana wa binadamu, nimekuweka kuwa mlinzi wa watu wa nyumba ya Israeli; unaposikia neno kutoka katika kinywa changu lazima uwape onyo langu.^b **8** Ni- napomwambia mtu mwovu, ‘Wewe mwovu, hakika utakufa!’^c lakini wewe humwonyi waziwazi mtu huyo mwovu ili abadili njia yake, yeye kwa kuwa ni mwovu atakufa kwa sababu ya kosa lake mwenyewe,^d lakini damu yake nitaidai kutoka kwako. **9** Lakini ukimwonya mtu mwovu aiache njia yake naye akatae kubadili njia yake, atakufa kwa sababu ya kosa lake,^e lakini wewe kwa hakika utauokoa uhai wako.*^f

10 “Na wewe, mwana wa binadamu, waambie hivi watu wa nyumba ya Israeli: ‘Ninyi mmesema hivi: “Maasi yetu na dhambi zetu zinatulemea sana na kutufanya tudhoofike;^g basi tunawezaje kuendelea kuishi?”^h **11** Waambie, “Kwa hakika kama ninavyoishi,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, “Mimi si-furahishwi na kifo cha mwovu,ⁱ bali kwamba mtu mwovu abadili njia yake^j na kuendelea kuishi.^k Geukeni, geukeni mziache njia zenu mbaya,^l kwa nini mfe, enyi watu wa nyumba ya Israeli?”^m

12 “Na wewe, mwana wa binadamu, waambie wana wa watu wako, ‘Uadilifu wa mtu mwadilifu hautamwoko akiasi;ⁿ wala uovu wa mwovu hautamkwaza akiacha uovu wake,^o wala hakuna mtu

33:6 *Au “nitamfanya mlinzi awajibike kwa sababu ya damu ya mtu huyo.”
33:9 *Au “utaikoa nafsi yako.”

32:30 *Au “kaburini.” **33:4** *Tnn., “kumwondoa.” **33:5** *Au “nafsi yake.”

yeyote mwadilifu atakayee-ndelea kuishi kwa sababu ya uadilifu wake siku atakayotenda dhambi.^a **13** Ninapomwambia mtu mwadilifu: “Hakika utaendelea kuishi,” naye autumaini uadilifu wake mwenyewe na kutenda kosa,^{*b} hakuna tendo lolote la uadilifu alilotenda litakalokumbukwa, lakini atakufa kwa sababu ya kosa alilotenda.^c

14 “Ninapomwambia mtu mwovu: “Hakika utakufa,” naye aiache dhambi yake na kutenda mambo ya haki na ya uadilifu,^d **15** na mtu huyo mwovu arudishe kitu kilichowekwa rehani^e na kulipa vitu alivyomnyang’anya mwingine,^f naye atembeke katika sheria za uzima kwa kutotenda kosa, hakika ataendelea kuishi.^g Hataakufu. **16** Hataadhibiwa kwa sababu ya dhambi yoyote aliyotenda.^{*h} Kwa hakika ataendelea kuishi kwa sababu ya kutenda mambo ya haki na ya uadilifu.ⁱ

17 “Lakini watu wako wamesema, ‘Njia ya Yehova si ya haki,’ ingawa kwa kweli ni njia yao isiyo ya haki.

18 “Mtu mwadilifu akiacha uadilifu wake na kutenda kosa, lazima afe kwa sababu ya kosa hilo.^j **19** Lakini mtu mwovu akiacha uovu wake na kutenda mambo ya haki na ya uadilifu, ataendelea kuishi kwa sababu ya kufanya hivyo.^k

20 “Lakini ninyi mnasema, ‘Njia ya Yehova si ya haki.’^l Nitamhukumu kila mmoja wenu kulingana na njia zake, enyi watu wa nyumba ya Israeli.”

33:13 *Au “kutenda jambo lisilo la haki.”

33:16 *Tnn., “Hakuna dhambi yoyote aliyotenda itakayokumbukwa.”

SURA YA 33

a Eze 18:26

b 2Pe 2:20

c Eze 18:4

d Isa 55:7
Eze 18:21
Mik 6:8

e Kut 22:26

f Law 6:2, 4
Eze 22:29g Law 18:5
Eze 18:27

h Isa 1:18

i Eze 20:11

j Ebr 10:38
2Pe 2:20

k Eze 18:27

l Eze 18:25, 29

Safu ya 2

a Eze 24:25-27

b 2Fa 25:4
2Nya 36:17
Yer 39:2

c Eze 3:26

d Yer 39:10
Eze 36:4

e Mwa 12:7

f Mwa 9:4
Law 17:12

g Eze 22:6

h Sef 3:3

i Yer 5:8

j Kum 4:26
Yos 23:15

21 Mwishowe katika mwaka wa 12, mwezi wa kumi, siku ya tano ya mwezi wa uhamisho wetu, mtu aliyetoroka Yerusalemu alinjia^a na kusema: “Jiji limeangamizwa!”^b

22 Basi, jioni ya siku iliyo-kuwa imetangulia kabla ya mtu huyo aliyetoroka kuja, mkono wa Yehova ulinjia naye akakifungua kinywa changu kabla ya mtu huyo kunijia asubuhi. Kinywa changu kilifunguliwa, nami sikuwa bubu tena.^c

23 Kisha neno la Yehova likanjia likisema: **24** “Mwana wa binadamu, wakaaji wa magofu^d haya wanasema hivi kuhusu nchi ya Israeli: ‘Abrahamu alikuwa mtu mmoja tu, hata hivyo aliimiliki nchi hii.^e Lakini sisi ni wengi; kwa hakika tumepewa nchi hii iwe mali yetu.’

25 “Kwa hivyo waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Mnakula chakula pamoja na damu,^f nanyi mnayainua macho yenu kwa sanamu zenu zinazochukiza* na kuendelea kumwaga damu.^g Basi kwa nini mwimiliki nchi hii? **26** Mmeutegemea upanga wenu.^h Mmetenda mambo yanayochukiza, na kila mmoja wenu amemchafua mke wa jirani yake.ⁱ Basi kwa nini mwimiliki nchi hii?”^j

27 “Unapaswa kuwaambia, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Kwa hakika kama ninavyoishi, wale wanaoishi katika magofu watauawa kwa upanga; na wale

33:25 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

walio uwanjani nitawafanya wawe chakula cha wanyama wa mwituni; na wale walio katika ngome na mapango watakuwa kwa ugonjwa.^a **28** Nitafanya nchi iwe mahame na ukiwa kabisa,^b na kiburi chake chenye majivuno kitakomeshwa, na milima ya Israeli itafanywa ukiwa,^c na hakuna yeyote atakayepitia humo. **29** Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapoifanya nchi iwe mahame na ukiwa kabisa^d kwa sababu ya mambo yote yanayochukiza ambayo wamefanya.”^e

30 “Na wewe, mwana wa binadamu, watu wako wanaoingia kukuhusu kando ya kuta na kwenye vizingiti vya milango ya nyumba.^f Kila mtu anamwambia ndugu yake, ‘Hebu njoo tusikie neno linalotoka kwa Yehova.’ **31** Watakusanyika na kuketi mbele yako kama watu wangu; nao watasikia maneno yako lakini hawatayatenda.^g Kwa maana wanakusifusifu kwa vinywa vyao* lakini moyo wao una pupa ya kupata faida isiyo ya haki. **32** Tazama! Kwao, wewe ni kama wimbo wa mapenzi, unaoimbwa kwa sauti tamu na kucheza kwa ustadi kwa kinanda. Watasi- kiamaneno yako, lakini hakuna yeyote atakayeyatenda. **33** Na yatakapotimia—kwa maana yatatimia—watalazimika kujua kwamba nabii alikuwa miongoni mwao.”^h

34 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, tabiri dhidi ya wachungaji wa

33:31 *Au “wanazungumza kwa tamaa sana.”

SURA YA 33

a Yer 42:22
Eze 5:12

b 2Nya 36:20, 21
Isa 6:11
Yer 44:2

c Eze 6:3

d Yer 9:11
Yer 25:11

e 2Fa 17:9
2Nya 36:14

f Yer 18:18

g Isa 29:13
Yer 44:16, 17

h Eze 2:5

Safu ya 2

SURA YA 34

a Yer 23:1
Mik 3:1, 11
Sef 3:3
Zek 11:17
Mt 23:13

b Isa 40:11
Yoh 21:15

c 2Fa 21:16
Yer 22:17
Mik 3:3
Zek 11:4, 5

d Isa 56:11

e Lu 15:4

f Yer 22:13

g Yer 23:2
Yer 50:6
Mt 9:36

Israeli. Tabiri, na uwaambie wachungaji hao, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Ole wao wachungaji wa Israeli,^a ambao wamekuwa wakijilisha wenyewe! Je, wachungaji hawapaswi kullisha kundi?”^b **3** Mnakula mafuta, mnajivika wenyewe sufu, nanyi mnamchinja mnyama aliyenona zaidi,^c lakini hamlishi kundi.’^d **4** Hamjawatia nguvu walio dhafu au kuwaponya wagonjwa au kuwafunga waliojeruhiwa au kuwarudisha waliotangatanga au kuwatafuta waliopotea;^e badala yake, mmewatawala kwa ukali na kwa uonevu.^f **5** Kwa hiyo walitawanyika kwa sababu hakukuwa na mchungaji;^g walitawanyika na kuwa chakula cha kila mnyama wa mwituni. **6** Kondoo wangu waliendelea kutangatanga kwenye milima yote na kwenye kila kilima kirefu; kondoo wangu walitawanyika kotekote duniani, na hakuna aliyewatafuta au kujitahidi kuwatafuta.

7 ““Kwa hiyo, ninyi wachungaji, lisikieni neno la Yehova: **8** “Kwa hakika kama ninavyoishi,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, “kwa sababu kondoo wangu wamekuwa windo, chakula cha kila mnyama wa mwituni, kwa sababu hapakuwa na mchungaji, nao wachungaji wangu hawakuwatafuta kondoo wangu; badala yake waliendelea kujilisha wenyewe, nao hawakuwalisha kondoo wangu.” **9** basi, ninyi wachungaji, lisikieni neno la Yehova. **10** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Niko dhidi ya wachungaji, nami nitafanya wawa-

jibike kwa sababu ya kondoo wangu,* nami nitawafukuza ili wasiwalishe[#] kondoo wangu,^a nao wachungaji hawatajilisha tena. Nitawaokoa kondoo wangu kutoka kinywani mwao, nao hawatakuwa chakula chao tena.”

11 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Mimi nipo hapa, na mimi mwenyewe nitawatafuta kondoo wangu na kuwatunza.^b **12** Nitawatunza kondoo wangu kama mchungaji ambaye amewapata kondoo wake waliotawanyika na kuwalisha.^c Nitawaokoa kutoka katika maeneo yote walikotawanyika siku ya mwingu na giza zito.^d **13** Nitawatoa katika mataifa na kuwakusanya pamoja kutoka katika nchi hizo na kuwaleta katika nchi yao na kuwalisha kwenye milima ya Israeli,^e kando ya vijito na kando ya makao yote nchini. **14** Nitawalisha kwenye malisho mazuri, na nchi ambamo watalisha itakuwa kwenye milima mirefu ya Israeli.^f Huko watalala katika nchi yote malisho mazuri,^g nao watakula kwenye malisho bora juu ya milima ya Israeli.”

15 ““Mimi mwenyewe nitawalisha kondoo wangu,^h na mimi mwenyewe nitawalaza,ⁱ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **16** “Aliyepotea nitamtafuta,^j anayetangatanga nitamrudisha, aliyejeruhiwa nitamfunga, na aliye dhaifu nitamtia nguvu; lakini aliyenona na aliye na nguvu nitamwangamiza. Huyu nitamlisha hukumu.”

34:10 *Au “nitadai kondoo wangu kutoka mikononi mwao.” #Au “wasiwachunge.”

SURA YA 34

a Yer 52:24-27

b 1Sa 17:34, 35
Zb 80:1
Isa 56:8

c Isa 40:11

d Yoe 2:1, 2
Sef 1:14, 15e Yer 23:3
Eze 11:17
Amo 9:14
Mik 7:14f Isa 25:6
Isa 30:23
Yer 31:12

g Yer 33:12

h Yer 3:15

i Sef 3:13

j Mik 4:6
Mt 15:24
Lu 15:4

Safu ya 2

a Zek 10:3

b Isa 40:11
Yer 23:3c Yoh 10:11
Ebr 13:20
1Pe 5:4
Ufu 7:17d Isa 11:1
Yer 30:9e Eze 37:24
Ho 3:5f Kut 29:45
Yer 31:1g Zb 2:6
Isa 9:6
Yer 23:5
Mik 5:2
Lu 1:32
Mdo 5:31

17 ““Kuwahusu ninyi kondoo wangu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Niko karibu kuhukumu kati ya kondoo mmoja na kondoo mwingine, kati ya kondoo dume na mbuzi dume.^a **18** Je, hamtosheki kujilisha kwenye malisho yaliyo bora zaidi? Je, ni lazima myakanyage-kanyage kwa miguu yenu malisho yenu mengine? Na baada ya kunywa maji yaliyo safi zaidi, je, ni lazima myachafue kwa kuyakanyaga-kanyaga kwa miguu yenu? **19** Je, kondoo wangu wanapaswa kujilisha kwa malisho mliyokanyagakanyaga kwa miguu yenu na kunywa maji yaliyochafuliwa kwa kukanyagwakanyagwa kwa miguu yenu?”

20 ““Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anawambia hivi: “Mimi nipo hapa, na mimi mwenyewe nitahukumu kati ya kondoo aliyenona na kondoo aliyekonda, **21** kwa maana kwa ubavu wenu na kwa bega lenu mliendelea kuwasukuma, na kwa pembe zenu mliendelea kuwasukuma wote waliokuwa wagonjwa mpaka mkawatawanya maeneo ya mbali. **22** Nami nitawaokoa kondoo wangu, nao hawataendelea kuwa windo;^b nami nitahukumu kati ya kondoo mmoja na kondoo mwingine. **23** Nami nitamweka mchungaji mmoja juu yao,^c mtumishi wangu Daudi,^d naye atawalisha. Yeye mwenyewe atawalisha na kuwa mchungaji wao.^e **24** Na mimi, Yehova, nitakuwa Mungu wao,^f na mtumishi wangu Daudi atakuwa kiongozi wao. Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.^g

25 ““Nitafanya agano la amani pamoja nao,^a na kuwandoa kabisa nchini wanyama hatari wa mwituni,^b ili wakae kwa usalama nyikani na kulala misituni.^c 26 Nitawafanya wao na eneo linalozunguka kilima changu kuwa baraka,^d nami nitaifanya mvua inyeshe kwa wakati unaofaa. Baraka zitamwagika kama mvua.^e 27 Miti ya shambani itazaa matunda yake, na udongo utatoa mazao yake,^f nao wataishi kwa usalama nchini. Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nita-kapozivunja nira zao^g na kuwaokoa kutoka mikononi mwa wale waliowafanya kuwa watumwa. 28 Hawatakuwa windo la mataifa tena, na wanyama wa mwituni wa dunia hawatawanyafua, nao wataishi kwa usalama, na hakuna mtu atakayewaogopesha.^h

29 ““Nitawatarishia shamba maarufu,^{*} nao hawataku-fa tena kwa njaa kali nchini,ⁱ na hawatafedhehesha tena na mataifa.^j 30 ‘Nao watalazimika kujua kwamba mimi, Yehova Mungu wao, niko pamoja nao na kwamba wao, watu wa nyumba ya Israeli, ni watu wangu,^k’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

31 “Nanyi kondoo wangu,^l kondoo ninaowatunza, ninyi ni wanadamu tu, nami ni Mungu wenu,[’] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

35 Neno la Yehova likanijia tena likisema: 2 “Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako kwenye eneo lenye milima la Seiri,^m na utabiri dhidi yake.ⁿ 3 Uliambie,

34:29 *Tnn., “ili wapate jina.”

SURA YA 34

a Eze 37:26

b Law 26:6

Isa 11:6-9

Isa 35:9

Isa 65:25

Ho 2:18

c Yer 23:6

Yer 33:16

d Isa 56:7

Eze 20:40

Mik 4:1

e Mwa 12:2, 3

Kum 28:12

Zek 8:13

f Law 26:4

Zb 85:12

Isa 35:2

Eze 36:30

g Law 26:13

h Yer 30:10

Yer 46:27

i Eze 36:29

j Eze 36:15

k Eze 37:27

l Zb 78:52

Zb 100:3

Isa 40:11

SURA YA 35

m Mwa 32:3

Kum 2:5

n Yer 49:8

Omb 4:22

Eze 25:8, 9

Oba 1

Safu ya 2

a Eze 25:12, 13

b Yoe 3:19

Mal 1:3

c Mwa 27:41

Amo 1:11

d Zb 137:7

Oba 10

e Oba 15

f Eze 25:14

g Eze 25:13

h Yer 49:17, 18

Eze 25:13

Mal 1:4

i Eze 36:5

Oba 13

‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Niko dhidi yako, ewe eneo lenye milima la Seiri, nami nitaunyoo-sha mkono wangu dhidi yako na kukufanya uwe mahame na ukiwa.^a 4 Nitafafanya majiji yako kuwa magofu, nawe utakuwa mahame na ukiwa;^b nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova. 5 Kwa maana ulikuwa na chuki isiyo na mwisho,^c nawe uliwatia Waisraeli mikononi mwa upanga wakati wa msiba wao, wakati wa adhabu yao ya mwisho.”^d

6 “‘Kwa hiyo, kwa haki-ka kama ninavyoishi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘nitakutayarisha kwa ajili ya umwagaji wa damu, na umwagaji wa damu utaku-fuatia.^e Kwa maana uliichukia damu, umwagaji wa damu utaku-fuatia.^f 7 Nitalifanya eneo lenye milima la Seiri kuwa mahame na ukiwa,^g nami nita-mwangamiza mtu yeyote anayepitia humo na yeyote anayeurudi. 8 Nitaijaza milima yake watu waliouawa; na wale waliouawa kwa upanga wataanguka kwenye vilima vyako, katika mabonde yako, na katika vijito vyako vyote. 9 Nita-kufanya uwe ukiwa wa kudu-mu, na majiji yako hayatakali-wa;^h nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’

10 “Kwa sababu ulisema, ‘Mataifa haya mawili na nchi hizi mbili zitakuwa zangu, nasi tutazimiliki zote mbili,ⁱ hata ingawa Yehova mwenyewe alikuwa humo, 11 ‘kwa hiyo kwa hakika kama ninavyoishi,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘nita-kutendea kulingana na hasira

ileile na wivu uleule ulioonyesha ulipowachukia;^a nami nitajijulisha miongoni mwao nitakapokuhukumu. **12** Kisha utalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimesikia mambo yote ya dharau uliyosema kuhusu milima ya Israeli, uliposema, “Imefanywa ukiwa nasi tumepewa ili tuinyafue.”* **13** Nanyi mlizungumza kwa kiburi dhidi yangu, na kuzidisha maneno yenu dhidi yangu.^b Niliyasiakia yote.’

14 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Dunia yote itashangilia nitakapokufanya uwe mahame na ukiwa. **15** Kama ulivyoshangilia urithi wa watu wa nyumba ya Israeli ulipofanywa ukiwa, hivyo ndivyo nitakavyokutendea.^c Utakuwa magofu yaliyo ukiwa, ewe eno lenye milima la Seiri, naam, Edomu yote;^d nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’”

36 “Nawe, mwana wa binaadamu, tabiri kuhusu milima ya Israeli, nawe useme, ‘Enyi milima ya Israeli, lisikieni neno la Yehova. **2** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Adui amesema hivi dhidi yenu, ‘Aha! Hata mahali pa juu pa zamani pamekuwa mali yetu!’”^e

3 “Basi tabiri, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Kwa sababu wamekufanya uwe ukiwa na kukushambulia kutoka kila upande, ili uwe mali ya wale waliookoka* kutoka kati ya mataifa na watu wanaendelea ku-

35:12 * Tnn., “tumepewa kama chakula.”
36:3 * Tnn., “waliobaki.”

SURA YA 35

a Amo 1:11

b Oba 3

c Omb 4:21
Oba 12, 15d Isa 34:5
Eze 25:12, 13
Eze 36:5

SURA YA 36

e Yer 49:1
Eze 35:10

Safu ya 2

a Kum 28:37
1Fa 9:7
Omb 2:15
Da 9:16

b Yer 25:9

c Zb 79:4
Eze 34:28

d Sef 3:8

e Oba 12

f Eze 25:12, 13
Eze 35:10, 11
Amo 1:11g Zb 74:10
Zb 123:4h Yer 25:9
Yer 49:17i Isa 44:23
Isa 51:3
Eze 36:30

zungumza kukuhusu na kuku-chongea,^a **4** kwa hiyo, enyi milima ya Israeli, sikieni neno la Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anavyoambia milima na vilima, vijito na mabonde, magofu yaliyofanywa ukiwa,^b na majiji yaliyoachwa ambayo yameporwa na kudhihakiwa na wale waliookoka kutoka katika mataifa yanayowazunguka;^c **5** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anawaambia hivi: ‘Katika moto wa bidii yangu^d nitawakemea wale waliookoka kutoka katika mataifa na nchi yote ya Edomu, wale ambao kwa shangwe nyingi na kwa dharau kubwa*^e wamechukua nchi yangu na kuifanya kuwa mali yao, ili wachukue mali shoyake na kuipora.’”^f

6 “Basi tabiri kuhusu nchi ya Israeli, nawe uiambie milima na vilima, vijito na mabonde, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Tazama! Nitazungumza kwa bidii yangu na kwa ghadhabu yangu, kwa sababu mmefedheshwa na mataifa.’”^g

7 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Mimi mwenyewe ninainua mkono wangu na kuapa kwamba mataifa yanayozunguka yatabeba aibu yao wenyewe.’^h **8** Lakini ninyi, enyi milima ya Israeli, mtachipusha matawi na kuzaa matunda yenu kwa ajili ya watu wangu Waisraeli,ⁱ kwa maana watarudi hivi karibuni. **9** Kwa maana niko pamoja nanyi, nami nitawageukia,

36:5 * Au “dharau katika nafsi.”

nanyi mtalimwa na kupandwa mbegu. **10** Nitazidisha idadi ya watu wako—nyumba yote ya Israeli, yote—nayo majiji yatakaliwa^a na magofu yatajengwa upya.^b **11** Naam, nitazidisha idadi ya watu wako na mifugo yako;^c wataongezeka na kuzaana. Nami nitafanya ukaliwe kama ilivyokuwa zamani,^d nami nitakufanya usitawi kuliko mwanzoni;^e nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.^f **12** Nitawafanya watu—watu wangu Waisraeli—watembe juu yako, nao watakumiliki.^g Utakuwa urithi wao, nawe hutawafanya wakose watoto tena kamwe.”^h

13 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kwa kuwa wanawaambia ninyi, “Wewe ni nchi inayowameza watu na kuwau watoto wa mataifa yako,”’ **14** ‘kwa hiyo, hutawameza tena watu wala kuyafanya mataifa yako yakose watoto,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **15** ‘Sitaruhusu tena utukanye na mataifa au udhihakiwe na watu,ⁱ nawe hutafanya tena mataifa yako yakwazike,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

16 Na neno la Yehova likanijia tena likisema: **17** “Mwana wa binadamu, watu wa nyumba ya Israeli walipokuwa wakiishi katika nchi yao, walilichafua kwa njia zao na matendo yao.^j Njia zao zilikuwa kama uchafu wa hedhi kwangu.^k **18** Basi nikawambagia ghadhabu yangu kwa sababu ya damu waliyoimwaga juu ya nchi^l na kwa sababu waliichafua nchi kwa sanamu

SURA YA 36

a Zek 8:4

b Isa 51:3
Yer 30:18, 19
Amo 9:14

c Yer 31:27

d Isa 54:7
Yer 30:18

e Hag 2:9

f Ho 2:20
Yoe 3:17g Yer 32:44
Oba 17

h Isa 65:23

i Isa 54:4
Isa 60:14
Mik 7:8
Sef 2:8
Sef 3:19j Zb 106:38
Isa 24:5
Yer 2:7
Yer 16:18k Law 12:2
Isa 64:6

l Isa 42:24, 25

Safu ya 2

a Eze 23:37

b Law 26:38
Eze 22:15c Isa 52:5
Ro 2:24d Zb 74:18
Isa 48:9
Eze 20:9

e Zb 106:7, 8

f Isa 5:16
Eze 20:41

g Zb 102:13-15

h Kum 30:3
Isa 43:5
Yer 23:3
Eze 34:13
Ho 1:11i Hes 19:13
Zb 51:7j Isa 4:4
Yer 33:8

zao zinazochukiza.*^a **19** Basi nikawatawanya miongoni mwa mataifa na kuwatawanya katika nchi mbalimbali.^b Niliwahukumu kulingana na njia yao na kulingana na matendo yao. **20** Lakini walipoingia katika mataifa hayo, watu walilichafua jina langu takatifu^c kwa kusema hivi kuwahu-su: ‘Hawa ndio watu wa Yehova, lakini walilazimika kutoka katika nchi yake.’ **21** Basi nitalihangaikia jina langu takatifu, ambalo watu wa nyumba ya Israeli walilichafua miongoni mwa mataifa ambako walienda.”^d

22 “Kwa hiyo, waambie watu wa nyumba ya Israeli, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Sifanyi jambo hili kwa ajili yenu, enyi watu wa nyumba ya Israeli, bali kwa ajili ya jina langu takatifu, ambalo ninyi mmelichafua miongoni mwa mataifa ambako mlienda.”’^e **23** ‘Kwa hakika nitalitakasa jina langu kuu,^f ambalo lilichafuliwa miongoni mwa mataifa, ambalo mlilichafua miongoni mwao; nayo mataifa yatalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova,’^g asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘nitakapotakaswa miongoni mwenu mbele ya macho yao. **24** Nitawatoa kutoka kwa mataifa na kuwakusanya kutoka katika nchi zote na kuwaleta katika nchi yenu.^h **25** Nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi;ⁱ nami nitawatakaswa kutokana na uchafu wenu^j wote na kutoka-

36:18 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

na na sanamu zenu zote zinazochukiza.^a **26** Nitawapa moyo mpya^b na kutia roho mpya ndani yenu.^c Nitauondoa moyo wa jiwe^d kutoka mwilini mwenu na kuwapa moyo wa nyama.* **27** Nitaitia roho yangu ndani yenu, nami nitawafanya mtembee katika masharti yangu,^e nanyi mtashika na kufuata sheria zangu.* **28** Kisha mtakaa katika nchi niliyowapa mababu zenu, nanyi mtakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu.^f

29 “Nitawaokoa kutokana na uchafu wenu wote na kuita nafaka na kuifanya iwe tele, nami sitawaletea njaa kali.^g **30** Nitayafanya matunda ya mti na mazao ya shamba yawe tele, ili msipatwe tena na aibu ya njaa kali miongoni mwa mataifa.^h **31** Kisha mtakumbuka njia zenu ovu na matendo yenu mabaya, nanyi mtajichukia kwa sababu ya hatia yenu na matendo yenu yanayochukiza.ⁱ **32** Lakini jueni jambo hili: Sifanyi hivyo kwa ajili yenu,^j asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Badala yake, aibikeni na kufedheheka kwa sababu ya njia zenu, enyi watu wa nyumba ya Israeli.’

33 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Siku nitakayowatakasa kutokana na hatia yenu yote, nitayafanya majiji yakaliwe^k na magofu yajengwe upya.^l **34** Nchi yenye ukiwa, iliyokuwa ukiwa ili kila mtu anayepita aione, italimwa. **35** Na watu watasema: “Nchi iliyoku-

36:26 *Yaani, moyo ulio mwepesi kutii mwongozo wa Mungu. **36:27** *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

SURA YA 36

a Eze 6:4

b Yer 32:39

c Zb 51:10
Eze 11:19, 20

d Zek 7:12

e Yer 31:33

f Yer 30:22
Eze 37:25, 27

g Eze 34:29

h Eze 34:27

i Ezi 9:6
Ne 9:26
Yer 31:18
Eze 6:9j Kum 9:5
Da 9:19

k Zek 8:8

l Isa 58:12
Yer 33:10, 11
Amo 9:14

Safu ya 2

a Mwa 2:8

b Isa 51:3

c Eze 28:26
Eze 37:14

d Kut 23:17

e Yer 30:18, 19

SURA YA 37

f Ufu 21:10

g Eze 37:11

h Kum 32:39
1Sa 2:6

wa ukiwa imekuwa kama bustani ya Edeni,^a na majiji yaliyokuwa magofu na yaliyokuwa ukiwa na kubomolewa sasa yana ngome na yanakaliwa na watu.”^b **36** Na mataifa yaliyobaki kukuzunguka yatalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimejenga kilichobomolewa, nami nimepanda kilichofanywa ukiwa. Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema, nami nimelitenda.’^c

37 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Nitawaruhusu pia watu wa nyumba ya Israeli waniombe nitwatende jambo hili: Nitazidisha idadi ya watu wao kama kundi. **38** Kama kundi la watu watakatifu, kama kundi la Yerusalemu* wakati wa sherehe zake,^d majiji yaliyokuwa magofu yatajaa makundi ya watu;^e nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.”

37 Mkono wa Yehova ulikuwa juu yangu, naye Yehova akanichukua kwa roho yake na kuniweka chini katikati ya bonde tambarare,^f nalo lilikuwa limejaa mifupa. **2** Akanizungusha kwenye mifupa hiyo yote, nami nikao-na kwamba kulikuwa na mifupa mingi sana katika bonde hilo tambarare, nayo ilikuwa mikavu sana.^g **3** Akaniuliza: “Mwana wa binadamu, je, mifupa hii inaweza kuwa hai?” Nikajibu: “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, wewe ndiye unayejua.”^h **4** Basi akaniambia: “Itabirie mifupa hii, uiambie, ‘Enyi mifupa mikavu, lisikieni neno la Yehova:

36:38 *Au labda, “Kama makundi ya kondoos wa dhabihu huko Yerusalemu.”

5 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ameiambia hivi mifupa hii: “Nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtakuwa hai.”^a 6 Nitaweka kano na nyama juu yenu, nami nitawafunika kwa ngozi na kutia pumzi ndani yenu, nanyi mtakuwa hai; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.””

7 Kisha nikatabiri kama nilivyoamriwa. Mara tu nilipotabiri, nikasikia sauti, sauti ya vitu vinavyogongana, nayo mifupa ikaanza kukaribiana, mfupa kwa mfupa. 8 Kisha nikaona kano na nyama zikija juu yake, na ngozi ikazifunika. Lakini bado hakukuwa na pumzi ndani yake.

9 Kisha akaniambia: “Utabirie upepo. Tabiri, mwana wa binadamu, nawe uambie upepo, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Njoo kutoka kwenye zile pepo nne, ewe upepo,* nawe uwapulizie watu waliouawa, ili wawe hai.””

10 Basi nikatabiri kama alivyoiamuru, nayo pumzi* ikaingia ndani yao, nao wakaanza kuishi na kusimama kwa miguu yao;^b walikuwa jeshi kubwa ajabu.

11 Kisha akaniambia: “Mwana wa binadamu, mifupa hii ni watu wote wa nyumba ya Israeli.^c Wanasema, ‘Mifupa yetu imekauka, nalo tumaini letu limepotea.^d Tumeangamizwa kabisa.’ 12 Basi tabiri uwaambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Nitayafungua makaburi yenu^e na kuwainua kutoka katika makaburi yenu, watu wa-

37:9 *Au “pumzi; roho.” 37:10 *Au “roho.”

SURA YA 37

a Mwa 2:7
Eze 37:14

b Ufu 11:11

c Eze 36:10

d Isa 49:14

e Isa 66:14

Safu ya 2

a Eze 11:17
Amo 9:14

b Zb 126:2

c Isa 32:14, 15
Eze 36:27

d 2Nya 15:9
2Nya 30:11

e 1Fa 11:31
1Fa 12:20

f Isa 11:13
Yer 3:18

g Yer 50:4
Zek 10:6

ngu, na kuwaleta katika nchi ya Israeli.^a 13 Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapoyafungua makaburi yenu na nitakapowainua kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu.”^b 14 ‘Nitaitia roho yangu ndani yenu,^c nanyi mtakuwa hai, nami nitawafanya mwishi katika nchi yenu; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimesema nami nimelitenda,’ asema Yehova.”

15 Neno la Yehova likanijia tena likisema: 16 “Nawe, mwana wa binadamu, chukua kijiti nawe uandike juu yake, ‘Kwa ajili ya Yuda na kwa ajili ya watu wa Israeli walio pamoja naye.’”^d Kisha uchukue kijiti kingine na kuandika juu yake, ‘Kwa ajili ya Yosefu, kijiti cha Efraimu, na watu wote wa nyumba ya Israeli walio pamoja naye.’”^e 17 Kisha viunganishe ili viwe kijiti kimoja tu mkononi mwako.^f 18 Watu wako* watakapokuuliza, ‘Je, hutatuambia mambo haya yanamaanisha nini?’ 19 waambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Nitakichukua kijiti cha Yosefu, kilicho mkononi mwa Efraimu, na makabila ya Israeli yaliyo pamoja naye, nami nitakiunganisha na kijiti cha Yuda; nami nitavifanya viwe kijiti kimoja,^g navyo vitakuwa kijiti kimoja mkononi mwangu.”” 20 Vijiti utakavyoandika juu yake vinapaswa kuwa mkononi mwako ili waviione.

21 “Kisha uwaambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova

37:16 *Au “wanaoshirikiana naye.” 37:18 *Tnn., “Wana wa watu wako.”

anasema hivi: “Nitawachukua Waisraeli kutoka katika mataifa ambako walienda, nami nitawakusanya pamoja kutoka kila upande na kuwaleta katika nchi yao.^a **22** Nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi hiyo,^b kwenye milima ya Israeli, na mfalme mmoja atawatawala wote,^c nao hawatakuwa tena mataifa mawili; wala hawatagawanyika tena kuwa falme mbili.^d **23** Hawatajitia unajisi tena kwa sanamu zao zinazochukiza* na kwa matendo yao yanayochukiza na kwa makosa yao yote.^e Nitawaokoa kutoka katika ukosefu wao wote wa uaminifu ambao umewafanya watende dhambi, nami nitawatakasaa. Watakuwa watu wangu, nami mwenyewe nitakuwa Mungu wao.^f

24 ““Mtumishi wangu Daudi atakuwa mfalme wao,^g na wote watakuwa na mchungaji mmoja.^h Watatembea katika sheria zangu* na kuzishika amri zangu kwa uangalifu.ⁱ **25** Wataishi katika nchi nliyompa mtumishi wangu, Yakobo, ambamo mababu zenu waliishi,^j nao watakaa humo milele,^k wao na watoto* wao na watoto wa watoto wao;^l na mtumishi wangu Daudi atakuwa kiongozi^m wao milele.^m

26 ““Nami nitafanya agano la amani pamoja nao;ⁿ litakuwa agano la milele pamoja nao. Nitawaimarisha na kuwafanya wawe wengi^o na kupaweka mahali pangu patakatifu miongoni mwao milele.

37:23 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau. **37:24** *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.” **37:25** *Tnn., “wana.” #Au “mkuu.”

SURA YA 37

- a Kum 30:3
Isa 11:12
Yer 16:14, 15
Amo 9:14
b Yer 3:18
Ho 1:11
c Mwa 49:10
Zb 2:6
Isa 9:6
Yer 23:5
Lu 1:32
d Eze 37:19
Zek 10:6
e Isa 2:18
Eze 11:18
Ho 14:8
Zek 13:2
f Yer 31:33
Eze 36:28
g Yer 23:5
Yer 30:9
Ho 3:5
Lu 1:32
h Yoh 10:16
1Pe 5:4
i Kum 30:8-10
Yer 32:39
Eze 36:27
j Yer 30:3
k Yoe 3:20
l Isa 60:21
Amo 9:15
m Eze 34:24
Lu 1:32
n Eze 34:25
o Yer 30:19
Zek 8:5

Safu ya 2

- a Law 26:12
Eze 11:19, 20
Eze 43:7
Ho 2:23
Ufu 21:3
b Eze 36:23

SURA YA 38

- c Eze 38:15
d Isa 66:19
Eze 27:13
Eze 32:26
e Eze 39:1
f 2Fa 19:20, 28
Eze 29:3, 4
Eze 39:2
g Eze 38:15
h 1Nya 1:8
i Mwa 10:2, 3
Eze 27:14
j Eze 39:2

27 Hema langu litakuwa* pamoja nao,[#] nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.^a **28** Na mataifa yata-lazimika kujua kwamba mimi, Yehova, ninawatakasaa Waisraeli mahali pangu patakatifu patakapokuwa kati yao milele.^{”””b}

38 Neno la Yehova likanijia tena likisema: **2** “Mwana wa binadamu, uelekeze uso wako dhidi ya Gogu wa nchi ya Magogu,^c kiongozi mkuu* wa Mesheki na Tubali,^d na utabiri dhidi yake.^e **3** Sema, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Tazama, niko dhidi yako, ewe Gogu, kiongozi mkuu* wa Mesheki na Tubali. **4** Nitaku-geuza na kutia kulabu katika mataya yako^f na kukutoa pamoja na jeshi lako lote,^g farasi na wapanda farasi, wote wakiwa wamevaa mavazi ya kifahari, kusanyiko kubwa sana lenye ngao kubwa na ngao ndogo,* wote wakiwa na mapanga; **5** Uajemi, Ethiopia, na Putu^h wako pamoja nao, wote wakiwa na ngao ndogo na kofia; **6** Gomeri na wanajeshi wake wote, watu wa nyumba ya Togarmaⁱ kutoka sehemu za mbali zaidi za kaskazini, pamoja na wanajeshi wake wote—mataifa mengi yako pamoja nawe.^j

7 ““Uwe tayari, ujitayari-she, wewe pamoja na majeshi yako yote yaliyokusanyika pamoja nawe, nawe utakuwa kamanda* wao.

37:27 *Au “Makao yangu yatakuwa; Nyumba yangu itakuwa.” #Au “juu yao.” **38:2, 3** *Au “mkuu wa wakuu.” **38:4** *Kwa kawaida ilibebwa na wapiga mishale. **38:7** *Tnn., “mlinzi.”

8 ““Utakaziwa fikira* baada ya siku nyingi. Katika miaka ya mwisho utaishambulia nchi ambayo watu wake wamerudishwa kutoka kwenye uharibifu wa upanga, waliokusanywa pamoja kutoka katika mataifa mengi, na kule-twa kwenye milima ya Israeli, ambayo kwa muda mrefu ilikuwa imebaki ukiwa. Wakaa-ji wa nchi hii walirudishwa kutoka katika mataifa, na wote wanakaa kwa usalama.^a 9 Utawashambulia kama dhoro-ba nawe utafunika nchi kama mawingu, wewe na wanajeshi wako wote na mataifa mengi pamoja nawe.”

10 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Siku hiyo mawazo yataingia moyoni mwako, nawe utapanga njama ya uovu. 11 Utasema: “Nitaivamia nchi yenye vijiji visivyo na ulinzi.”^b Nita-washambulia wale wanaokaa kwa usalama, bila usumbufu, wote wanaoishi katika vijiji visivyolindwa na ukuta, makomeo, au malango.” 12 Ili ku-pora na kuchukua nyara nyingi, ili kushambulia maeneo yaliyoharibiwa ambayo sasa yanakaliwa na watu^c walio-kusanywa kutoka katika mataifa,^d ambao wanajikusanyia utajiri na mali,^e wale wanaoishi katikati ya dunia.

13 “Sheba^f na Dedani,^g wafanyabiashara wa Tarshishi^h na mashujaa* wake wote watakuuliza: “Je, unavamia ili upore na kupata nyara nyingi? Je, umekusanya majeshi yako ili kubeba fedha na

38:8 *Au “Utaitwa.” 38:11 *Au “eneo lililo wazi la mashambani.” 38:13 *Au “wanasimba wenye manyoya marefu shingoni.”

SURA YA 38

a Yer 23:5, 6
Eze 28:25, 26
Eze 34:25

b Kut 15:9

c Yer 33:12

d Zek 10:8

e Isa 60:5
Isa 61:6

f Eze 27:22

g Eze 27:15

h Eze 27:25

Safu ya 2

a Eze 38:8

b Eze 39:2

c Sef 3:8

d Yoe 3:2

e Kut 14:4
2Fa 19:17-19
Zb 83:17, 18
Eze 39:21

f Yoe 3:16
Nah 1:2
Zek 2:8

dhahabu, kuchukua utajiri na mali, ili kuteka nyara nyingi sana?”

14 “Basi tabiri, mwana wa binadamu, nawe umwambie Gogu, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Siku ambayo watu wangu Waisraeli watakapokuwa wakiishi kwa usalama, je, hutajua jambo hilo?”^a 15 Utakuja kutoka mahali pako, kutoka sehemu za mbali zaidi za kaskazini,^b wewe pamoja na mataifa mengi, wote wakiwa wamepanda farasi, kusanyiko kubwa, jeshi kubwa sana.^c 16 Kama mawingu yanayoifunika nchi, utawashambulia watu wangu Waisraeli. Katika kipindi cha mwisho cha zile siku, nitakuleta uishambulia nchi yangu^d ili mataifa yanijue nitakapojitakasa mwenyewe kupitia wote mbele ya macho yao, ewe Gogu.”^e

17 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Je, wewe si yuleyule niliyesema kumhusu katika siku za zamani kupitia watumishi wangu manabii wa Israeli, waliotabiri kwa miaka mingi kwamba utaletwa ili kuwashambulia?’

18 ““Siku hiyo, siku ambayo Gogu ataishambulia nchi ya Israeli,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘ghadhabu yangu kali itawaka.^f 19 Kwa bidii yangu, kwa moto wa ghadhabu yangu, nitazungumza; na siku hiyo kutakuwa na tetemeko kubwa la ardhi katika nchi ya Israeli. 20 Kwa sababu yangu, samaki wa baharini, ndege wa angani, wanyama wa mwituni, wanyama wote wanaotambaa juu ya nchi, na wanadamu wote walio dunia-ni watatetemeka, nayo milima

itaangushwa chini,^a na miamba itaanguka, na kila ukuta utaporomoka.’

21 “Nitauita upanga umshambulie kwenye milima yangu yote,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Upanga wa kila mtu utamshambulia ndugu yake mwenyewe.’^b

22 Nitamletea hukumu yangu* kwa ugonjwa hatari^c na kwa umwagaji wa damu; nami nitaleta dhidi yake mvua kubwa ya mafuriko na mawe ya mvua^d na moto^e na kiberiti^f na dhidi ya wanajeshi wake na dhidi ya mataifa mengi yaliyo pamoja naye.^g **23** Nami hakika nitajitukuza na kujitakasa na kujijulisha mwenyewe mbele ya macho ya mataifa mengi; nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.’

39 “Nawe, mwana wa binaadamu, tabiri dhidi ya Gogu,^h umwambie, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Niko dhidi yako, Gogu, kiongozi mkuu* wa Meshaki na Tubali.’ **2** Nitakugeza na kukuongoza na kukufanya uje kutoka sehemu za mbali zaidi za kaskazini/ na kukuleta kwenye milima ya Israeli. **3** Nitaupiga upinde wako utoke kwenye mkono wako wa kushoto na kufanya mishale yako ianguke kutoka kwenye mkono wako wa kulia. **4** Utaanguka kwenye milima ya Israeli,^k wewe na wanajeshi wako wote na mataifa yatakayokuwa pamoja nawe. Nitakufanya uwe chakula cha kila aina ya ndege wanaowinda na wanyama wa mwituni.”^l

38:22 *Au “Nitamhukumu.” 39:1 *Au “mkuu wa wakuu.”

SURA YA 38

a Nah 1:5

b 2Nya 20:23
Hag 2:22
Zek 14:13

c Zek 14:12

d Kut 9:22
Yos 10:11

e Isa 30:30

f Mwa 19:24

g Yer 25:31

SURA YA 39

h Eze 38:2

i Eze 27:13
Eze 32:26

j Eze 38:4, 15

k Eze 38:21

l Ufu 19:17, 18

Safu ya 2

a Yer 25:33

b Eze 38:22

c Eze 38:16

d Isa 6:3

e Zb 46:9

f Eze 38:2

5 “‘Utaanguka uwanjani,^a kwa maana mimi mwenyewe nimesema,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

6 “‘Nami nitatuma moto dhidi ya Magogu na dhidi ya wale wanaokaa visiwani kwa usalama,^b nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova. **7** Nitalifanya jina langu takatifu lilulikane miongoni mwa watu wangu Waisraeli, nami sitaruhusu jina langu takatifu lichafuliwe tena; na mataifa yatalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova,^c Mtaakatifu katika Israeli.’^d

8 “‘Naam, jambo hilo linakuja, nalo litatendeka,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Hiyo ndiyo siku ambayo nimesema kuhusu. **9** Kwa hakika wakaaaji wa majiji ya Israeli watoka nje na kuwasha moto kwa silaha—ngao ndogo* na ngao kubwa, pinde na mishale, rungu za vita[#] na mikuki. Nao watazitumia kuwasha moto^e kwa miaka saba. **10** Hawatahitaji kukusanya kuni shambani wala kuokota kuni misituni, kwa sababu watatumia silaha hizo kuwasha mioto.’

“Watawateka nyara wale waliowateka nyara na kuwapora wale waliokuwa wakiwapora,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

11 “‘Siku hiyo, nitampa Gogu^f kaburi katika Israeli, kwenye bonde la wale wanaosafiri upande wa mashariki wa bahari, nalo litazuia njia ya wale wanaopitia humo. Hapo ndipo watakapomzika Gogu na umati wake wote, nao

39:9 *Kwa kawaida ilibebwa na wapi-ga mishale. [#]Au labda, [#]silaha zenye ncha kali zilizovaliwa mkononi.”

wataliita Bonde la Hamon-Gogu.*^a **12** Kwa miezi saba watu wa nyumba ya Israeli watawazika ili kuitakasa nchi.^b **13** Watu wote wa nchi watafan-nya kazi ya kuwazika, na hilo litawaletea umaarifu siku nitakayojitukuza,^c asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

14 Watu watapewa kazi ya kupitapita nchini daima na kuzika miili iliyobaki juu ya dunia, ili kuitakasa dunia. Wataendelea kutafuta kwa miezi hiyo saba. **15** Wale wanaopitapita nchini watakapoona mfupa wa mwanadamu, wataweka alama kando yake. Kisha wale waliopewa kazi ya kuzika watauzika mfupa huo katika Bonde la Hamon-Gogu.^d **16** Na huko pia kutakuwa na jiji linaloitwa Hamona.* Nao wataitakasa nchi.^e

17 “Nawe, mwana wa binaadamu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Waambie ndege wa kila aina na wanyama wote wa mwituni, “Kusanyikeni pamoja na mje. Kusanyikeni kuzunguka dhabihu yangu ninayowatayarishia, dhabihu kubwa kwenye milima ya Israeli.^f Mtakula nyama na kunywa damu.^g **18** Mtakula nyama ya wenyewe nguvu na kunywa damu ya viongozi wa dunia—kondoo dume, wanakondoo, mbuzi, na ng’ombe dume—wanyama wote waliononeshwa wa Bashani. **19** Mtakula mafuta kwa pupa mpaka mshibe na kunywa damu mpaka mlewe kutokana na dhabihu nitakayowatayarishia.”

20 “Mtashibishwa mezani pangu kwa farasi na waende-

39:11 *Au “Bonde la Umati wa Gogu.”
39:16 *Maana yake “Umati.”

SURA YA 39

a Eze 39:15

b Kum 21:22, 23

c Eze 38:16

d Eze 39:11

e Eze 39:12

f Isa 34:6-8
Yer 46:10
Sef 1:7

g Ufu 19:17, 18

Safu ya 2

a Eze 38:4-6
Hag 2:22
Ufu 19:17, 18b Kut 7:4
Kut 14:4
Isa 37:20
Eze 38:16
Mal 1:11

c 2Nya 7:21, 22

d Kum 31:18
Isa 59:2e Law 26:24, 25
Kum 32:30
Zb 106:40, 41f Yer 30:3
Eze 34:13g Ho 1:11
Zek 1:16

h Eze 36:21

i Da 9:16

j Law 26:5, 6

k Yer 30:10
Amo 9:14
Sef 3:20l Isa 5:16
Eze 36:23

shaji wa magari, watu wenye nguvu na kila aina ya mashujaa,^a asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

21 “Nitauonyesha wazi utukufu wangu kati ya mataifa, nayo mataifa yote yataona hukumu ambayo nimetekeleza na nguvu nilizoonyesha* kati yao.^b **22** Kuanzia siku hiyo, watu wa nyumba ya Israeli watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao. **23** Nayo mataifa yatalazimika kujua kwamba watu wa nyumba ya Israeli walipelekwa uhamishoni kwa sababu wa kosa lao, kwa sababu hawakuwa waaminifu kwangu.^c Basi niliwaficha uso wangu^d na kuwatia mikononi mwa maadui wao,^e na wote wakauawa kwa upanga. **24** Niliwatendea kulingana na uchafu wao na makosa yao, nami nikawaficha uso wangu.’

25 “Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Nitawarudisha watu wa Yakobo waliotekwa^f na kuwaonyesha rehema watu wote wa nyumba ya Israeli;^g nami nitalitetea jina langu takatifu kwa bidii.^{*h} **26** Baada ya kufedheheshwa kwa sababu ya ukosefu wao wote wa uaminifu kunielekea,ⁱ watakaa kwa usalama katika nchi yao, na hakuna mtu atakayewaogopesha.^j **27** Nitakapowarudisha kutoka katika mataifa na kuwakusanya pamoja kutoka katika nchi za maadui wao,^k mimi pia nitajitakasa miongoni mwao mbele ya macho ya mataifa mengi.’^l

39:21 *Tnn., “mkono nilioonyesha.”
39:25 *Tnn., “nitajitoka kikamili kwa ajili ya jina langu takatifu.”

28 “Watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao nitakapowapeleka uhamishoni miongoni mwa mataifa na kuwarudisha katika nchi yao, bila kumwacha yeyote kati yao huko.^a 29 Sitawaficha uso wangu tena,^b kwa maana nitawamiminia roho yangu watu wa nyumba ya Israeli,^c asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

40 Katika mwaka wa 25 wa uhamisho wetu,^d mwanzoni mwa mwaka, siku ya 10 ya mwezi, katika mwaka wa 14 baada ya jiji kuanguka,^e siku hiyohiyo mkono wa Yehova ulikuwa juu yangu, naye akanipeleka jijini.^f 2 Kupitia maono kutoka kwa Mungu, alinileta katika nchi ya Israeli na kuniweka juu ya mlima mrefu sana,^g na juu yake kulikuwa na jengo lililoonekana kama jiji, upande wa kusini.

3 Aliponipeleka huko, niliona mtu fulani ambaye alionekana kama shaba.^h Alikuwa na kamba ya kitani na utete wa kupimia* mkononi mwake,ⁱ naye alikuwa amesimama langoni. 4 Mtu huyo akaniaambia: “Mwana wa binadamu, tazama kwa uangalifu, sikiliza kwa makini, na ukazie fikira* kila kitu ninachokuonyesha, kwa maana uliletwa hapa kwa sababu hiyo. Waambie watu wa nyumba ya Israeli kila kitu unachooona.”^j

5 Nikaona ukuta uliozunguka nje ya hekalu.* Mkononi

40:3 *Angalia Nyongeza B14. 40:4 *Tnn., “uweke moyo wako kwa.” 40:5 *Tnn., “nyumba.” Neno “hekalu” linatumiwa katika sura ya 40-48 wakati ambapo linarejelea majengo ya hekalu au hekalu lenyewe.

SURA YA 39

a Kum 30:4

b Isa 45:17
Isa 54:8
Yer 29:14

c Isa 32:14, 15
Yoe 2:28

SURA YA 40

d 2Fa 24:15, 16

e 2Fa 25:8-10
Eze 33:21

f Eze 8:3

g Isa 2:2

h Eze 1:5, 7
Da 10:5, 6

i Eze 47:3
Zek 2:1, 2
Ufu 11:1
Ufu 21:15

j Eze 43:10

Safu ya 2

a Eze 40:10
Eze 43:1, 4
Eze 46:1, 2

b 1Nya 9:26, 27

mwa mtu huyo kulikuwa na utete wa kupimia wenye urefu wa mikono sita (kila mkono ulikuwa umeongezwa urefu wa kiganja kimoja).^{*} Akaaanza kupima ukuta, nao ulikuwa na unene wa utete mmoja na urefu wake ulikuwa utete mmoja.

6 Kisha akaja kwenye lango lililotazama mashariki^a na kupanda ngazi zake. Alipopima kizingiti cha lango hilo, upana wake ulikuwa utete mmoja, na upana wa kile kizingiti kingine ulikuwa utete mmoja pia. 7 Kila chumba cha walenzi kilikuwa na urefu wa utete mmoja na upana wa utete mmoja, na kulikuwa na kipimo cha mikono mitano kati ya vyumba vya walenzi.^b Kipimo cha kizingiti cha lango kando ya ukumbi wa lango linalotazama upande wa ndani kilikuwa utete mmoja.

8 Alipima ukumbi wa lango kuelekea ndani, nao ulikuwa utete mmoja. 9 Kisha akapima ukumbi wa lango, nao ulikuwa mikono minane; na akapima nguzo zake za pembeni, nazo zilikuwa mikono miwili; na ukumbi wa lango ulikuwa upande uliotazama ndani.

10 Kulikuwa na vyumba vitatu vya walenzi katika kila upande wa lango la mashariki. Vyumba hivyo vitatu vilikuwa na ukubwa uleule, nazo nguzo za pembeni zilizokuwa pande zote mbili zilikuwa na ukubwa uleule.

11 Kisha akapima upana wa lango, nao ulikuwa mikono 10;

40:5 *Tnn., “utete wa kupimia wa mikono sita, mkono mmoja na kiganja kimoja.” Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14.

na urefu wa lango ulikuwa mikono 13.

12 Eneo lililogawanywa lililokuwa mbele ya vyumba vya walenzi kila upande lilikuwa na kipimo cha mkono mmoja. Vyumba vya walenzi pande zote mbili vilikuwa mikono sita kila kimoja.

13 Kisha akapima lango kutoka kwenye paa la chumba kimoja cha mlinzi* mpaka kwenye paa la kile kingine, na upana wake ulikuwa mikono 25; mlango mmoja ulitazamana na mlango mwingine.^a

14 Kisha akapima nguzo za pembeni, ambazo zilikuwa na urefu wa mikono 60, pia nguzo za pembeni katika malango kuzunguka ua. **15** Urefu kutoka upande wa mbele wa lango mpaka mbele ya ukumbi upande wa ndani wa lango ulikuwa mikono 50.

16 Ndani ya lango, kila upande kwenye vyumba vya walenzi na pia kwenye nguzo zake za pembeni kulikuwa na madirisha yenye viunzi ambavyo ukubwa wake ulipungua kutoka nje kwenda ndani.^b Upande wa ndani wa kumbi ulikuwa pia na madirisha kila upande, na kulikuwa na michongo ya mitende^c kwenye nguzo za pembeni.

17 Kisha akanileta kwenye ua wa nje, nami nikaona vyumba vya kulia chakula,^{*d} na sakafu iliyozunguka ua. Kulikuwa na vyumba 30 vya kulia chakula kwenye ile sakafu. **18** Urefu wa sakafu iliyokuwa kando ya malango ulikuwa sawa na urefu wa malango—hiyo ilikuwa sakafu ya chini.

40:13 *Labda inarejelea sehemu ya juu ya ukuta wa chumba cha mlinzi. **40:17** *Au "nikaona vyumba."

SURA YA 40

a Eze 40:20, 21

b 1Fa 6:4
Eze 41:26

c 1Fa 6:35

d 1Nya 28:12

Safu ya 2
a Eze 41:20, 26

b Eze 46:9

c Eze 40:20, 22

19 Kisha akapima umbali* kutoka mbele ya lango la chini mpaka kwenye uzio wa ua wa ndani. Ulikuwa mikono 100 upande wa mashariki na wa kaskazini.

20 Ua wa nje ulikuwa na lango lililotazama kaskazini, naye akapima urefu wake na upana wake. **21** Kulikuwa na vyumba vitatu vya walenzi kila upande. Nguzo zake za pembeni na ukumbi wake ulikuwa na vipimo sawa na lile lango la kwanza. Urefu wake ulikuwa mikono 50 na upana wake mikono 25.

22 Madirisha yake, ukumbi wake, na michongo yake ya mitende^a yalikuwa na ukubwa ulio sawa na yale ya lango la mashariki. Watu wangeweza kuyafikia kwa kupanda ngazi saba, na ukumbi wake ulikuwa mbele yake.

23 Kulikuwa na lango kati ka ua wa ndani lililotazamana na lango la kaskazini na lingine lililotazamana na lango la mashariki. Alipima urefu kutoka lango moja hadi lingine, nao ulikuwa mikono 100.

24 Kisha akanileta upande wa kusini, nami nikaona lango upande wa kusini.^b Akapima nguzo zake za pembeni na ukumbi wake, nazo zilikuwa na ukubwa ulio sawa na zile nyingine. **25** Kila upande na pia katika ukumbi wake kulikuwa na madirisha, kama madirisha yale mengine. Urefu wake ulikuwa mikono 50 na upana wa mikono 25. **26** Kulikuwa na ngazi saba zilizoelekea langoni,^c na ukumbi wake ulikuwa mbele yake. Nalo lili-

40:19 *Tnn., "upana."

kuwa na michongo ya mitende kwenye nguzo zake za pembeni, mmoja kila upande.

27 Ua wa ndani ulikuwa na lango lililotazama upande wa kusini, akapima kuelekea kusini kutoka lango moja mpa-ka lingine, na urefu wake ulikuwa mikono 100. **28** Kisha akanileta kwenye ua wa ndani kupitia lango la kusini; alipolipima lango la kusini, lilikuwa na ukubwa sawa na yale malango mengine. **29** Vyumba vyake vya walinzi, nguzo zake za pembeni, na ukumbi wake ulikuwa na ukubwa sawa na malango mengine. Kulikuwa na madirisha kila upande na pia kwenye ukumbi. Urefu wake ulikuwa mikono 50 na upana wake mikono 25.^a **30** Kulikuwa na kumbi pande zote; zilikuwa na urefu wa mikono 25 na upana wa mikono 5. **31** Ukumbi wake ulitazama ua wa nje, na kulikuwa na michongo ya mitende kwenye nguzo zake za pembeni,^b na ngazi nane zilielekea kwenye lango hilo.^c

32 Aliponileta kwenye ua wa ndani kutoka mashariki, alilipima lango, nalo lilikuwa na ukubwa sawa na malango mengine. **33** Vyumba vyake vya walinzi, nguzo zake za pembeni, na ukumbi wake ulikuwa na ukubwa sawa na malango mengine, na kulikuwa na madirisha kila upande na pia kwenye ukumbi. Urefu wake ulikuwa mikono 50 na upana wake mikono 25. **34** Ukumbi wake ulitazama ua wa nje, na kulikuwa na michongo ya mitende kwenye nguzo zake mbili za pembeni, na ngazi nane zilielekea kwenye lango hilo.

SURA YA 40

a Eze 40:20, 21

b Eze 40:16

c Eze 40:32, 34
Eze 40:35, 37

Safu ya 2

a Eze 44:4

b Law 8:21

c Law 1:3, 6
Law 8:20
Eze 43:18

d Law 4:3, 4

e Law 5:6
Law 7:1
Eze 42:13
Eze 44:29

35 Kisha akanileta kwenye lango la kaskazini^a naye akalipima; ukubwa wake ulikuwa sawa na malango mengine.

36 Vyumba vyake vya walinzi, nguzo zake za pembeni, na ukumbi wake ulikuwa sawa na malango mengine. Lango hilo lilikuwa na madirisha kila upande. Urefu wake ulikuwa mikono 50 na upana wa mikono 25. **37** Nguzo zake za pembeni zilitazama ua wa nje na kulikuwa na michongo ya mitende kwenye nguzo zake mbili za pembeni, na ngazi nane zilielekea kwenye lango hilo.

38 Kulikuwa na chumba cha kulia chakula pamoja na mlango wake karibu na nguzo za pembeni za malango, mahali ambapo dhabihu nzima za kuteketewa zilioshewa.^b

39 Kulikuwa na meza mbili kila upande wa ukumbi wa lango ambapo wanyama wa dhabihu nzima za kuteketewa walichinjwi,^c na wa dhabihu za dhambi,^d na wa dhambi za hatia.^e **40** Kwenye njia inayopanda kuelekea katika lango la kaskazini, kulikuwa na meza mbili nje ya lango. Kulikuwa pia na meza mbili upande ule mwingine wa ukumbi wa lango. **41** Kulikuwa na meza nne kila upande wa lango—meza nane kwa ujumla—ambapo wanyama wa dhabihu walichinjwi.

42 Zile meza nne za dhabihu nzima za kuteketewa zilitengenezwa kwa mawe yaliyochongwa. Zilikuwa na urefu wa mkono mmoja na nusu, upana wa mkono mmoja na nusu, na kimo cha mkono mmoja. Juu yake waliweka vifaa vilivyotumiwa kuwachinjia wanyama wa dhabihu za

kuteketezwa na dhahibu nyingine. **43** Rafu zenye upana wa kiganja kimoja, zilifungwa kuzunguka pande zote za kuta za ndani; na nyama za dhahibu za zawadi ziliwekwa kwenye zile meza.

44 Kulikuwa na vyumba vya kulia chakula vya waimbaji nje ya lango la ndani;^a vilikuwa katika ua wa ndani karibu na lango la kaskazini, vikitazama upande wa kusini. Kulikuwa na chumba kine cha kulia chakula karibu na lango la mashariki, kilitazama kaskazini.

45 Akaniambia: “Chumba hiki cha chakula kinachotazama upande wa kusini ni cha makuhani walio na jukumu la kutimiza utumishi wa hekaluni.^b **46** Chumba cha kulia chakula kinachotazama upande wa kaskazini ni cha makuhani walio na jukumu la kutimiza utumishi wa madhabahu.^c Hao ni wana wa Sadoki,^d Walawi waliopewa kazi ya kumkaribia Yehova ili kumhudumia.”^e

47 Kisha akapima ua wa ndani. Ulikuwa na urefu wa mikono 100 na upana wa mikono 100, mraba. Madhabahu ilikuwa mbele ya hekalu.

48 Kisha akanileta kwenye ukumbi wa hekalu,^f naye akapima nguzo ya pembeni ya ukumbi, nayo ilikuwa mikono mitano upande mmoja na mikono mitano upande wa pili. Upana wa lango ulikuwa mikono mitatu upande mmoja na mikono mitatu upande wa pili.

49 Ukumbi ulikuwa na urefu wa mikono 20 na upana wa mikono 11.* Watu walipanda

40:49 *Au labda, “12.”

SURA YA 40

a 1Nya 6:31, 32

b Hes 3:6-8
1Nya 9:22, 23
Zb 134:1

c Law 6:12, 13
Hes 18:5
2Nya 13:10, 11

d 1Fa 2:35
Eze 43:19

e Hes 16:39, 40
Eze 44:15, 16

f 1Fa 6:3
2Nya 3:4

Safu ya 2

a 1Fa 7:21

SURA YA 41

b 1Fa 6:20
2Nya 3:8

c Kut 26:33

d 1Fa 6:5

ngazi ili kufika kwenye ukumbi huo. Kulikuwa na nguzo kwenye miimo ya pembeni, nguzo moja kila upande.^a

41 Kisha akanileta kwenye sehemu ya nje ya patakatifu,^{*} naye akapima nguzo za pembeni; zilikuwa na upana wa mikono sita[#] upande mmoja na mikono sita upande mwingine. **2** Mlango ulikuwa na upana wa mikono kumi, na kuta za pembeni za mlango zilikuwa mikono mitano upande mmoja na mikono mitano upande wa pili. Akapima urefu wake, ambao ulikuwa mikono 40, na upana wake, mikono 20.

3 Kisha akaingia ndani^{*} na kupima nguzo ya pembeni ya mlango, nayo ilikuwa na unene wa mikono miwili, na mlango ulikuwa na upana wa mikono sita. Kuta za pembeni za mlango zilikuwa[#] mikono saba. **4** Kisha akapima chumba kilichotazamana na sehemu ya nje ya patakatifu, na urefu wake ulikuwa mikono 20, na upana wake mikono 20.^b Naye akaniambia: “Hapa ndipo Patakatifu Zaidi.”^c

5 Kisha akapima ukuta wa hekalu, na unene wake ulikuwa mikono sita. Na vyumba vya kando kuzunguka hekalu vilikuwa na upana wa mikono minne.^d **6** Vyumba vya kando vilikuwa na ghorofa tatu, moja juu ya nyingine, na kila

41:1 *Tnn., “hekalu.” Katika sura ya 41 na 42, neno hili linamaanisha sehemu ya nje ya mahali patakatifu (Patakatifu) au sehemu yote ya mahali patakatifu (hekalu kutia ndani Patakatifu na Patakatifu Zaidi). #Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14. 41:3 *Yaani, kwenye sehemu ya ndani ya mahali patakatifu, au Patakatifu Zaidi. #Tnn., “upana wa mlango ulikuwa.”

ghorofa ilikuwa na vyumba 30. Kulikuwa na vidato kuzunguka pande zote za ukuta wa hekalu ambavyo vilishikilia vyumba vya kando, ili vishikio visiguye ukuta wa hekalu lenyewe.^a **7** Pande zote mbili za hekalu zilikuwa na njia ili-yopindapinda* ambayo ilipanuka kadiri ilivyopanda kuelekea vyumba vya juu.^b Upana uliongezeka kutoka ghorofa moja hadi nyingine kadiri mtu alivyopanda kutoka ghorofa ya chini hadi ya juu aki-pitia ghorofa ya katikati.

8 Nikaona kwamba kulikuwa na jukwaa lililoinuliwa kuzunguka hekalu, na misingi ya vyumba vya kando ilikuwa na urefu wa utete mmoja wa mikono sita mpaka kwenye pembe. **9** Upana wa ukuta wa nje wa vyumba vya kando ulikuwa mikono mitano. Kulikuwa na eneo lililo wazi* kando ya vyumba vya kando vilivyokuwa sehemu ya hekalu.

10 Kati ya hekalu na vile vyumba vya kulia chakula*^c kulikuwa na eneo lenye upana wa mikono 20 kila upande. **11** Kulikuwa na mlango kati ya vyumba vya kando na eneo lililo wazi lililokuwa upande wa kaskazini na mlango mwingine upande wa kusini. Upana wa eneo lililo wazi ulikuwa mikono mitano pande zote.

12 Jengo lililokuwa magharibi likitazama eneo lililo wazi lilikuwa na upana wa mikono 70 na urefu wa mikono 90; ukuta wa jengo hilo ulikuwa na unene wa mikono mitano pande zote.

41:7 *Inaonekana inarejelea ngazi za duara. 41:9 *Inaonekana ni njia nye-mbamba iliyozunguka hekalu. 41:10 *Au "vile vyumba."

SURA YA 41

a 1Fa 6:6, 10

b 1Fa 6:8

c 1Nya 28:12

Safu ya 2

a 2Nya 3:8
Eze 41:4

b 1Fa 6:4

c 1Fa 6:15
2Nya 3:5d 1Fa 6:29
1Fa 7:36
2Nya 3:7

e Eze 40:16

f Eze 1:5, 10
Ufu 4:7

13 Akapima hekalu, nalo lilikuwa na urefu wa mikono 100. Lile eneo lililo wazi, jengo,* na kuta zake zilikuwa pia na urefu wa mikono 100.

14 Upana wa upande wa mbele wa hekalu uliotazama mashariki na pia wa eneo lililo wazi ulikuwa mikono 100.

15 Akapima urefu wa jengo lililotazama eneo lililo wazi upande wa nyuma, pamoja na mabaraza yake pande zote mbili, na urefu wake ulikuwa mikono 100.

Pia akapima sehemu ya nje ya patakatifu, sehemu ya ndani ya patakatifu,^a na zile kumbi za ua, **16** pia vizingiti, madirisha yenye viunzi ambavyo ukubwa wake ulipungua kutoka nje kwenda ndani,^b na mabaraza yaliyokuwa katika sehemu hizo tatu. Karibu na kizingiti kulikuwa na mbao^c zilizofunika kuta kuanzia sakafuni mpaka kwenye madirisha; nayo madirisha yalikuwa yamefunikwa.

17 Pia alipima sehemu ya juu ya mlango na sehemu ya ndani ya hekalu na nje na kuzunguka ukuta wote. **18** Kulikuwa na michongo ya make-rubi^d na pia michongo ya mitende,^e kila mtende ulikuwa kati ya makerubi wawili, na kila kerubi alikuwa na nyuso mbili. **19** Uso wa mwana-damu ulitazama mtende upande mmoja, na uso wa simba* ulitazama mtende upande wa pili.^f Ilichongwa hivyo katika hekalu lote. **20** Kuanzia sakafuni mpaka sehemu

41:13 *Yaani, jengo la upande wa magharibi wa mahali patakatifu. 41:19 *Au "mwanasimba mwenye manyoya marefu shingoni."

iliyo juu ya mlango kulikuwa na michongo ya makerubi na michongo ya mitende kwenye ukuta wa patakatifu.

21 Miimo ya milango* ya patakatifu ilikuwa mraba.^a Mbele ya mahali patakatifu[#] kulikuwa na kitu kama **22** madhabahu ya mbao^b iliyokuwa na kimo cha mikono mitatu, na urefu wa mikono miwili. Ilikuwa na nguzo za pembeni, na sehemu yake ya chini* na kuta zake zilitengezwa kwa mbao. Kisha akaniambia: "Hii ndiyo meza iliyo mbele za Yehova."^c

23 Kulikuwa na milango miwili katika sehemu ya nje ya patakatifu na pia mahali patakatifu.^d **24** Milango ilikuwa na bawaba mbili zilizozunguka, bawaba mbili kwa kila mlango. **25** Kulikuwa na michongo ya makerubi na michongo ya mitende kwenye milango ya patakatifu, kama ile iliyokuwa ukutani.^e Pia kulikuwa na kifuniko* cha mbao juu ya upande wa mbele wa ukumbi kwa nje. **26** Pia kulikuwa na madirisha yenye viunzi ambavyo ukubwa wake ulipungua kutoka nje kwenda ndani^f na michongo ya mitende pande zote mbili za ukumbi, pia kwenye vyumba vya kando vya hekalu na vifuniko.

42 Kisha akanipeleka kwenye ua wa nje kuelekea kaskazini.^g Naye akanileta kwenye jengo lenye vyumba vya kulia chakula lililopakana na eneo lililo wazi,^h upande

41:21 *Tnn., "Mwimo wa mlango." Inaonekana maneno haya yanarejelea njia ya kuingia Patakatifu. [#]Inaonekana inarejelea Patakatifu Zaidi. **41:22** *Tnn., "urefu wake." **41:25** *Au "paa dogo."

SURA YA 41

a 1Fa 6:33

b Kut 30:1
1Fa 7:48
Ufu 8:3c Eze 44:16
Mal 1:7

d 1Fa 6:31-35

e Eze 41:17, 18

f Eze 40:16

SURA YA 42

g Eze 40:2

h Eze 42:13

Safu ya 2

a Eze 41:12, 15

b Eze 41:10

c Eze 42:10, 11

wa kaskazini wa jengo linalofuata.^a **2** Urefu wake katika mlango wa kaskazini ulikuwa mikono 100,^{*} na upana wake mikono 50. **3** Lilikuwa kati ya ua wa ndani, ambao ulikuwa na upana wa mikono 20,^b na sakafu ya ua wa nje. Mabaraza yake yalitazamana na yalikuwa na urefu wa ghorofa tatu. **4** Mbele ya vyumba vya kulia chakula* kulikuwa na njia ya ndani^c yenye upana wa mikono 10 na urefu wa mikono 100,[#] na milango yake ilitazama kaskazini. **5** Vyumba vya kulia chakula vilivyokuwa juu katika jengo hilo vilikuwa vyembamba kuliko vile vya chini na vya katikati, kwa sababu mabaraza yalichukua nafasi kubwa ya vyumba hivyo. **6** Kwa maana mabaraza yalikuwa na urefu wa ghorofa tatu, lakini hayakuwa na nguzo kama nguzo za nyua. Ndiyo sababu nafasi kubwa zaidi ya vyumba vilivyokuwa juu ilichukuliwa na mabaraza kuliko katika ghorofa ya chini na ya katikati.

7 Ukuta wa nje wa mawe uliokuwa karibu na vyumba vya kulia chakula kuelekea ua wa nje uliotazama vile vyumba vingine vya kulia chakula ulikuwa na urefu wa mikono 50. **8** Kwa maana urefu wa vyumba vya kulia chakula vilivyotazama ua wa nje ulikuwa mikono 50, lakini vile vilivyotazama patakatifu vilikuwa na urefu wa mikono 100.

42:2 *Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14. **42:4** *Au "vile vyumba." [#]Kulingana na *Septuaginta* ya Kigiriki ni "urefu wa mikono 100." Maandishi ya Kiebrania yanasema hivi: "Njia ya mkono mmoja." Angalia Nyongeza B14.

9 Kulikuwa na njia iliyoelekea kwenye vyumba vya kulia chakula upande wa mashariki kutoka kwenye ua wa nje.

10 Kulikuwa pia na vyumba vya kulia chakula katika* ukuta wa mawe wa ua upande wa mashariki, karibu na eneo lililo wazi na pia jengo.^a

11 Mbele ya vyumba hivyo kulikuwa na njia kama ile ya vyumba vya kulia chakula vya kaskazini.^b Vyumba hivyo vilikuwa na urefu na upana uleule, na milango yake ya kutokea na ramani yake ililingana na ya vyumba vya kaskazini vya kulia chakula. Milango yake **12** ilikuwa kama milango ya vyumba vya kusini vya kulia chakula. Kulikuwa na mlango mahali ambapo njia ilianza, kabla ya ukuta wa mawe uliokuwa upande wa mashariki, mahali ambapo mtu angeweza kuingilia.^c

13 Kisha akaniambia: “Vyumba vya kulia chakula vya kaskazini na vyumba vya kulia chakula vya kusini vina vyopakana na eneo lililo wazi^d ndivyo vyumba vya kulia chakula vilivyo vitakatifu ambamo makuhani wanaomkaribia Yehova hula matoleo matakatifu zaidi.^e Matoleo matakatifu zaidi, toleo la nafaka, dhahihu ya dhambi, na dhahihu ya hatia huwekwa humo, kwa sababu mahali hapo ni patakatifu.^f **14** Makuhani wanapoingia, hawapaswi kutoka mahali patakatifu na kwenda kwenye ua wa nje kabla hawajavua mavazi wanayovaa wanapohudumu,^g kwa sababu ni matakatifu. Watavaa mavazi mengine ili waende ka-

42:10 *Tnn., “katika upana wa.”

SURA YA 42

a Eze 41:12
Eze 42:1

b Eze 42:4

c Eze 42:9

d Eze 42:1

e Law 6:14, 16
Law 7:1, 6
Law 10:12, 13
Law 24:8, 9
Hes 18:10
Eze 40:46

f Law 2:3
Hes 18:9
Ne 13:5

g Kut 28:40
Kut 29:8, 9
Law 8:13
Eze 44:19

Safu ya 2

a Eze 40:6

b Eze 40:5

c Eze 45:1, 2

d Law 10:10
Eze 44:23
2Ko 6:17

SURA YA 43

e Eze 40:6
Eze 42:15
Eze 44:1

f Eze 9:3
Eze 11:23

g Eze 1:24
Yoh 12:28, 29

h Isa 6:3
Eze 10:4

tika maeneo ambayo watu wanaruhusiwa kuingia.”

15 Alipomaliza kupima sehemu ya ndani ya hekalu,* akanipeleka nje kupitia lango linalotazama mashariki,^a naye akapima eneo hilo lote.

16 Akapima upande wa mashariki kwa ule utete wa kupimia.* Ulikuwa na urefu wa tete 500 kutoka upande mmoja hadi mwingine, kulingana na utete wa kupimia.

17 Akapima upande wa kaskazini, nao ulikuwa na urefu wa tete 500, kulingana na utete wa kupimia.

18 Akapima upande wa kusini, nao ulikuwa na urefu wa tete 500, kulingana na utete wa kupimia.

19 Akazunguka upande wa magharibi. Akapima urefu wa tete 500 kwa utete wa kupimia.

20 Akapima pande nne za eneo hilo. Lilikuwa na ukuta uliolizunguka pande zote^b uliokuwa na urefu wa tete 500 na upana wa tete 500,^c ili kutenganisha kitu kitakatifu na kitu cha matumizi ya kawaida.^d

43 Kisha akanipeleka kwenye lango linalotazama mashariki.^e **2** Hapo nikaona utukufu wa Mungu wa Israeli ukija kutoka mashariki,^f na sauti yake ilikuwa kama sauti ya maji yenye kishindo;^g nayo dunia iling'aa kwa utukufu wake.^h **3** Mambo niliyoona yalikuwa kama maono niliyoona nilipokuja* ku-liangamiza jiji, na yalionekana kama mambo niliyoona

42:15 *Tnn., “nyumba ya ndani.”
42:16 *Angalia Nyongeza B14. 43:3 *Au labda, “alipokuja.”

karibu na mto Kebari;^a nami nikaanguka kifudifudi.

4 Kisha utukufu wa Yehova ukaingia hekaluni* kupitia langu lililotazama mashariki.^b

5 Ndipo roho ikaniinua na ku-ningiza kwenye ua wa ndani, nami nikaona kwamba hekalu lilikuwa limejaa utukufu wa Yehova.^c **6** Kisha nikasikia mtu akizungumza nami kutoka katika lile hekalu, na mtu huyo akaja na kusimama kando yangu.^d **7** Akaniambia:

“Mwana wa binadamu, hapa ndipo mahali pa kiti changu cha ufalme^e na mahali pa nyayo za miguu yangu,^f ambapo nitakaa kati ya watu wa Israeli milele.^g Watu wa nyumba ya Israeli hawatalichafua tena jina langu takatifu,^h wao na wafalme wao, kwa ukahaba wao wa kiroho na kwa maiti za wafalme wao wanapokufa. **8** Kwa kuweka kizingiti chao kando ya kizingiti changu na mwimo wa mlango wao kando ya mwimo wa mlango wangu, kukiwa na ukuta tu kati yangu nao,ⁱ walilichafua jina langu takatifu kwa mambo yanayochukiza waliyotenda hivi kwa mba nikawaangamiza kabisa kwa hasira yangu.^j **9** Basi sasa na wauweke mbali nami ukahaba wao wa kiroho na maiti za wafalme wao, nami nitakaa miongoni mwao milele.^k

10 “Na wewe, mwana wa binadamu, waeleze watu wa nyumba ya Israeli kuhusu hekalu ili waaibike kwa sababu ya makosa yao,^m nao wapaswa kuichunguza ramani yake.* **11** Ikiwa wataaibi-

43:4 *Tnn., “kwenye ile nyumba.”
43:10 *Tnn., “kupima kielelezo chake.”

SURA YA 43

a Eze 1:3, 4
Eze 3:23

b Eze 10:19
Eze 44:1, 2

c Kut 40:34
1Fa 8:10
Eze 44:4

d Eze 40:3

e Isa 6:1
Yer 3:17
Eze 1:26

f 1Nya 28:2

g Kut 29:45
Zb 68:16
Zb 132:14
Yoe 3:17

h Eze 39:7
Zek 13:2

i Eze 8:3

j Da 9:12

k Eze 37:23
Eze 37:26
2Ko 6:16

l Eze 40:4

m Eze 16:63

Safu ya 2

a Eze 44:5

b Eze 11:19, 20
Eze 36:27

c Zb 93:5
Eze 40:2
Eze 42:20

d Kut 27:1
2Nya 4:1

e Kut 27:2
Ufu 9:13

ka kwa sababu ya mambo yote ambayo wamefanya, unapaswa kuwaonyesha ramani ya hekalu, mpangilio wake, na njia zake za kutokea, na za kuingilia.^a Waonyeshe ramani zake zote na maagizo yake, ramani zake na sheria zake, nawe uziandike mbele ya macho yao, ili waone ramani zake zote na kufuata maagizo yake.^b **12** Hii ndiyo sheria ya hekalu. Eneo lote kuzunguka juu ya mlima ni takatifu zaidi.^c Tazama! Hii ndiyo sheria ya hekalu.

13 “Hivi ndivyo vipimo vya madhabahu kwa kipimo cha mikono^d (kila mkono uliongezwa kiganja kimoja).^e Sehemu yake ya chini ni mkono mmoja na upana wake mkono mmoja. Ina ukingo ambao upana wake ni shubiri^f moja kuzunguka pembeni. Hiyo ndiyo sehemu ya chini ya madhabahu. **14** Kuanzia sehemu ya chini ya sakafu mpaka kwenye kidato cha chini kinachozunguka pande zote ni mikono miwili, na upana wake ni mkono mmoja. Kuanzia kidato kidogo kinachozunguka pande zote mpaka kwenye kidato kikubwa kinachozunguka pande zote ni mikono minne, na upana wake ni mkono mmoja. **15** Jiko la madhabahu lina urefu wa mikono minne, na kutoka kwenye jiko la madhabahu kuelekea juu kuna zile pembe nne.^e **16** Jiko la madhabahu ni la mraba, urefu wake ni miko-

43:13 *Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14. ^fYaani, upana wa kiganja cha mkono kuanzia kidole gumba hadi kidole kidogo, karibu sentimita 22.2 (inchi 8.75). Angalia Nyongeza B14.

no 12 na upana wake ni mikono 12.^a **17** Pande nne za kidato kinachozunguka zina urefu wa mikono 14 na upana wa mikono 14; na ukingo unaozunguka ni nusu mkono, na sehemu yake ya chini ni mkono mmoja pande zote.

“Na ngazi zake zinatazama upande wa mashariki.”

18 Kisha akaniambia: “Mwana wa binadamu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Hii ndiyo miongozo ya kufuata madhabahu inapotengenezwa, ili dhabihu nzima za kuteketezwa zitolewe na damu inyunyizwe juu yake.’^b

19 “Utawapa makuhani Walawi wazao wa Sadoki^c wanaonikaribia ili kunihudumia ng’ombe dume mchanga wa kundi kwa ajili ya dhabihu ya dhambi,^d’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **20** ‘Unapaswa kuchukua kiasi fulani cha damu yake na kuitia kwenye zile pembe nne za madhabahu, juu ya ncha nne za kidato kinachozunguka pande zote, na juu ya ukingo unaozunguka pande zote, ili kuitakasa kutokana na dhambi na kufunika dhambi yake.^e **21** Kisha utamchukua yule ng’ombe dume mchanga, ile dhabihu ya dhambi, ili umteketeze mahali palipochaguliwa pa hekalu, nje ya patakatifu.^f **22** Katika siku ya pili utatoa mbuzi dume ambaye hana kasoro kwa ajili ya dhabihu ya dhambi; nao wataitakasa madhabahu kutokana na dhambi kama walivyoitakasa kutokana na dhambi kwa kutumia yule ng’ombe dume mchanga.’

SURA YA 43

a Kut 38:1
2Nya 4:1

b Kut 40:29
Law 1:5
Law 8:18-21
Eze 45:19

c Eze 40:46
Eze 44:15
Eze 48:11

d Kut 29:10
Law 8:14

e Kut 29:36, 37
Law 8:15
Ebr 9:23

f Kut 29:14
Law 8:17
Ebr 13:11

Safu ya 2

a Law 2:13

b Kut 29:35

c Law 9:1

d Eze 20:40

SURA YA 44

e Eze 43:1

f Eze 46:1

g Eze 43:2

h Kum 12:5, 7

23 “Utakapomaliza kuitakasa kutokana na dhambi, utatoa ng’ombe dume mchanga wa kundi ambaye hana kasoro na kondoo dume wa kundi ambaye hana kasoro. **24** Nawe utawaleta kwa Yehova, na makuhani watawanyunyizia chumvi^a na kuwatoa kwa Yehova wakiwa dhabihu nzima ya kuteketezwa. **25** Kwa siku saba utamtoa mbuzi dume kwa ajili ya dhabihu ya dhambi kila siku,^b pia ng’ombe dume mchanga wa mifugo, na kondoo dume kutoka katika kundi; utawatoa wanyama ambao hawana kasoro.* **26** Kwa siku saba watafunika dhambi ya madhabahu, nao wataitakasa na kuiweka tayari. **27** Baada ya siku hizo kwisha, siku ya nane^c na kuendelea, kuhani atatoa dhabihu zenu* nzima za kuteketezwa na dhabihu za ushirika kwenye madhabahu; nami nitafurahishwa nanyi,^d asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.”

44 Akanirudisha kupitia lango la nje la patakatifu lililotazama mashariki,^e nalo lilikuwa limefungwa.^f **2** Ndipo Yehova akaniambia: “Lango hili litabaki likiwa limefungwa. Halipaswi kufunguliwa, na hakuna mwadamu yeyote atakayelitumia kuingia; kwa maana mimi Yehova, Mungu wa Israeli, nimeingia kupitia lango hilo,^g basi linapaswa kubaki likiwa limefungwa. **3** Hata hivyo, kiongozi ataketi humo ili ale mkate mbele zangu mimi Yehova,^h kwa maana

43:25 *Au “walio kamili.” 43:27 *Yaini, za watu.

yeye ni kiongozi. Ataingia kupitia ukumbi wa lango, naye atatoka kupitia lango hilo.”^a

4 Kisha akanileta kupitia lango la kaskazini mpaka mbele ya hekalu. Nilipotazama nikaona kwamba utakufu wa Yehova ulikuwa umejaa katika hekalu la Yehova.^b Basi nikaanguka chini kifudufudi.^c

5 Ndipo Yehova akaniambia: “Mwana wa binadamu, kaza fikira,* angalia, na usikilize kwa makini nitakayokuambia kuhusu maagizo na sheria za hekalu la Yehova. Tazama kwa makini sana njia ya kuingia hekaluni na njia zote za kutokea patakatifu.”^d **6** Utawaambia hivi watu wa nyumba ya Israeli walioasi: ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Matendo yenu yanayochukiza yametosha, enyi watu wa nyumba ya Israeli.

7 Mnapowaleta patakatifu pangu wageni ambao hawajatahiriwa moyoni na mwilini, wanalitua unajisi hekalu langu. Mnaotoa mkate wangu, mafuta, na damu, huku agano langu likivunjwa kwa sababu ya mateendo yenu yote yanayochukiza. **8** Hamjavitunza vitu vyangu vitakatifu.^e Badala yake mnawapa wengine majukumu ya kuhudumu mahali pangu patakatifu.”

9 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Hakuna mgeni yeyote anayeshi Israeli ambaye hajatahiriwa moyoni na mwilini atakayeingia mahali pangu patakatifu.”

10 “Lakini Walawi walio tangatanga na kwenda mbali nami^f Waisraeli waliponiacha

44:5 *Tnn., “elekeza moyo wako.”

SURA YA 44

a Eze 46:2

b Isa 6:1-3
Eze 10:4

c Eze 1:27, 28
Eze 3:23

d Eze 40:4

e Law 22:2
Hes 18:2, 3

f 2Fa 23:8, 9
2Nya 29:1, 5
Ne 9:34
Yer 23:11
Eze 8:5

Safu ya 2

a 1Nya 26:1

b Isa 9:16
Mal 2:8

c Hes 18:2, 4

d 1Fa 2:35
Eze 40:46

e Eze 48:9, 11

f Law 3:14-16

g Law 17:6

ili kufuata sanamu zao zinazochukiza* watapata madhara ya kosa lao. **11** Nao watakuwa wahudumu wa mahali pangu patakatifu ili kusimamia malango ya hekalu^a na kuhudumu hekaluni. Watawachinja wanyama wa dhabihu nzima za kuteketezwa na dhabihu kwa ajili ya watu, nao wata simama mbele ya watu ili kuwahudumia. **12** Kwa sababu waliwahudumia mbele ya sanamu zao zinazochukiza nao wakawa kikwazo na kuwafanya watu wa nyumba ya Israeli watende dhambi,^b ndiyo sababu nimeinua mkono wangu dhidi yao na kuapa,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, ‘nao watapata madhara ya kosa lao. **13** Hawatanikaribia ili kunitumikia wakiwa makuhani wangu wala kukaribia kitu chochote kati ya vitu vyangu vitakatifu au vitu vitakatifu kabisa, nao watabeba aibu yao kwa sababu ya mambo yenye kuchukiza waliyofanya. **14** Lakini nitawapa kazi ya kushughulikia majukumu ya hekalu, kushughulikia utumishi wa hekaluni na mambo yote yanayopaswa kufanywa humo.’^c

15 “‘Nao makuhani Walawi, wana wa Sadoki,^d walioshughulikia majukumu ya mahali pangu patakatifu Waisraeli waliponiacha,^e watanikaribia ili kunihudumia, nao wata simama mbele zangu ili kunitolea mafuta^f na damu,^g asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **16** ‘Hao ndio watakoingia mahali pangu patakatifu, nao wataikaribia meza

44:10 *Huenda neno la Kiebrania linahusiana na neno “mavi,” nalo hutumiwa kuonyesha dharau.

yangu ili kunihudumia,^a nao watatimiza majukumu yangu.^b

17 “Wanapoingia kwenye malango ya ua wa ndani, wanapaswa kuvaa mavazi ya kitani.^c Hawapaswi kuvaa vazi lolote la sufu wanapohudumu katika malango ya ua wa ndani au wakiwa ndani. **18** Wanapaswa kuvaa vilemba vya kitani kichwani, nao wanapaswa kuvaa suruali fupi za kitani viunoni mwao.^d Hawapaswi kuvaa chochote kitakachofanya watokwe na jasho. **19** Kabla ya kwenda kwenye ua wa nje—ua wa nje mahali palipo na watu—wanapaswa kuyavua mavazi waliyokuwa wamevaa walipokuwa wakihudumu^e na kuyaweka katika vyumba vitakatifu vya kulia chakula.^{*f} Kisha watavaa mavazi mengine, ili wasije wakawapitishia watu utakatifu^g kwa mavazi hayo. **20** Hawapaswi kunyoa kichwa chao^g au kuacha nywele za kichwa chao ziwe ndefu. Wanapaswa kupunguza nywele za vichwa vyao. **21** Makuhani hawapaswi kunywa divai wanapoingia kwenye ua wa ndani.^h **22** Hawapaswi kumwoa mjane au mwanamke aliyetalikiwa;ⁱ lakini wanaweza kumwoa bikira wa uzao wa Israeli au mjane wa kuhani.^j

23 “Wanapaswa kuwafundisha watu wangu tofauti kati ya kitu kitakatifu na kitu cha kawaida; nao watawafundisha tofauti kati ya kitu kisicho safi na kitu kilicho safi.^k **24** Wanapaswa kuwa waamuzi katika kesi;^l ni lazima wahukumu kulingana na sheria

44:19 *Au “vile vyumba vitakatifu.”
*Tnn., “wasije wakawatakasa watu.”

SURA YA 44

a Eze 41:21, 22

b Hes 18:7

c Kut 28:39, 42
Kut 39:27, 28
Law 16:4

d Kut 28:40, 42

e Law 6:10
Eze 42:14

f Eze 42:13

g Law 21:1, 5
Kum 14:1

h Law 10:9

i Law 21:7

j Law 21:10, 14

k Mal 2:7

l Kum 17:9

Safu ya 2

a 1Nya 23:3, 4
2Nya 19:8

b Law 23:2

c Law 21:1-3

d Law 4:3

e Hes 18:20
Kum 18:1
Yos 13:14
Eze 45:4

f Law 2:3

g Law 6:17, 18
Law 7:1, 6
1Ko 9:13h Law 27:21
Hes 18:14i Kut 23:19
Hes 18:8, 12
Hes 18:26, 27
Kum 18:4j Hes 15:20
Ne 10:35-37k Met 3:9, 10
Mal 3:10l Kut 22:31
Law 22:3, 8

SURA YA 45

m Yos 14:1, 2
Eze 47:21, 22

zangu.^{*a} Wanapaswa kufuata sheria zangu na amri zangu zinazohusu sherehe zangu zote^b na kuzitakasa sabato zangu. **25** Hawapaswi kumkaribia mwanadamu yeyote aliyekufa, la sivyo hawatakuwa safi. Hata hivyo, wanaweza kujichafua kwa ajili ya baba, mama, mwana, binti, au dada yao ambaye hajaolewa.^c **26** Na baada ya kuhani kutakasa, wanapaswa kumhesabia siku saba. **27** Siku anayoingia katika mahali patakatifu, katika ua wa ndani, ili kuhudumu katika mahali patakatifu anapaswa kutoa dhahibu yake ya dhambi,^d asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

28 “Na huu ndio utakaokuwa urithi wao: Mimi ndiye urithi wao.^e Msiwape mali yoyote katika Israeli, kwa maana mimi ndiye mali yao. **29** Wao ndio watakaokula toleo la nafaka,^f dhahibu ya dhambi, na dhahibu ya hatia,^g na kila kitu kilichotolewa katika Israeli kitakuwa chao.^h **30** Matunda yote ya kwanza yaliyo bora na kila aina ya mchango mta-kaotoa utakuwa wa makuhani.ⁱ Nanyi mnapaswa kumpatia kuhani mavuno ya kwanza ya unga wenu ambao haujakobolewa.^j Hilo litafanya baraka ikae juu ya nyumba zenu.^k **31** Makuhani hawapaswi kula ndege yeyote au mnyama yeyote aliyepatikana amekufa au kuraruliwa vipande vipande.^l

45 “Mtakapoigawa nchi iwe urithi,^m mnapaswa kumtolea Yehova sehemu takatifu ya nchi kuwa

44:24 *Tnn., “maamuzi yangu ya hukumu.”

mchango.^a Inapaswa kuwa na urefu wa mikono 25,000,* na upana wa mikono 10,000.^b Eneo hilo lote litakuwa[#] sehemu takatifu. **2** Ndani yake kutakuwa na eneo la mraba la mahali patakatifu lenye urefu wa mikono 500 na upana wa mikono 500,^{*c} na kila upande litakuwa na malisho yenye kipimo cha mikono 50.^d **3** Na kutoka katika kipimo hicho utapima urefu wa 25,000 na upana wa 10,000, na ndani yake kutakuwa na mahali patakatifu, kitu kitakatifu kabisa. **4** Litakuwa sehemu takatifu ya nchi kwa ajili ya makuhani,^e wahudumu wa mahali patakatifu, wanaokaribia ili kumhudumia Yehova.^f Patakuwa mahali kwa ajili ya nyumba zao, na mahali patakatifu kwa ajili ya patakatifu.

5 “Walawi, wahudumu wa hekaluni, watakuwa na sehemu yenye urefu wa mikono 25,000 na upana wa mikono 10,000,^g nao watamiliki vyumba 20 vya kulia chakula.^{*h}

6 “Mnapaswa kutoa sehemu ya jiji yenye urefu wa mikono 25,000 (inayolingana na mchango mtakatifu) na upana wa mikono 5,000.ⁱ Itakuwa ya watu wote wa nyumba ya Israeli.

7 “Na kwa ajili ya kiongozi kutakuwa na ardhi pande zote mbili za ule mchango mtakatifu na eneo lililogawiwa jiji. Itapakana na ule mchango mtakatifu na eneo la jiji. Itakuwa upande wa magha-

45:1 *Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14. #Au “Sehemu yote iliyo ndani ya mipaka hiyo itakuwa.” 45:2 *Tnn., “500 kwa 500.” 45:5 *Au “vyumba 20.”

SURA YA 45

a Eze 48:20

b Eze 48:8, 9

c Eze 42:20

d Yos 21:1, 2

e Eze 48:10, 11

f Eze 40:46

g Eze 48:13

h Eze 40:17

i Eze 48:15

Safu ya 2

a Eze 48:21

b Isa 32:1
Isa 60:17
Yer 22:17
Yer 23:5
Eze 22:27
Eze 46:18
Mik 3:1-3

c Yos 11:23

d Yer 22:3
Mik 6:8
Zek 8:16

e Mik 2:2

f Law 19:36
Met 11:1
Amo 8:5
Mik 6:10, 11

g Kut 30:13

ribi na upande wa mashariki. Urefu wake kuanzia mpaka wa magharibi hadi mpaka wa mashariki utakuwa sawa na mjawapo ya sehemu za makabila.^a **8** Ardhi hii itakuwa mali yake katika Israeli. Nao viongozi wangu hawatawatesa tena watu wangu,^b nao watawapa nchi watu wa nyumba ya Israeli kulingana na makabila yao.^c

9 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Imetoshia, enyi viongozi wa Israeli!’

“Acheni ukatili na ukandamizaji, na mtende mambo ya haki na ya uadilifu.^d Acheni kuchukua kwa nguvu mali ya watu wangu,^e asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

10 ‘Mnapaswa kutumia mizani sahihi na kipimo sahihi cha efa* na kipimo sahihi cha bathi.^{*f} **11** Kunapaswa kuwa na kipimo hususa cha efa na cha bathi. Kipimo cha bathi kinapaswa kuwa sehemu ya kumi ya homeri* na kipimo cha efa kinapaswa kuwa sehemu ya kumi ya homeri. Homeri ndiyo itakayokuwa kiwango cha kupimia.

12 Shekeli*^g inapaswa kuwa gera 20.* Na shekeli 20 ukijumlisha na shekeli 25 na pia shekeli 15, jumla yake itakuwa mane[#] moja kwako.’

13 “‘Huu ndio mchango unaopaswa kutoa: sehemu ya sita ya efa kutoka katika kila homeri ya ngano, na sehemu ya sita ya efa kutoka katika kila homeri ya shayiri. **14** Posho ya mafuta inapaswa kupimwa kwa kipimo cha ba-

45:10-12 *Angalia Nyongeza B14. 45:12 #Au “mina.” Angalia Nyongeza B14.

thi. Bathi ni sehemu ya kumi ya kori* na bathi kumi ni homeri moja, kwa sababu bathi kumi zinalingana na homeri moja. **15** Na kutoka katika kundi la mifugo ya Waisraeli, kondoo mmoja anapaswa kutolewa kwa kila kondoo 200. Hawa watatolewa kwa ajili ya toleo la nafaka,^a dhabihu nzima ya kuteketezwa,^b na dhabihu za ushirika,^c ili kufunika dhambi za watu,^d asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

16 “Watu wote nchini watatoa mchango huu^e kwa kiongozi wa Israeli. **17** Lakini kiongozi atakuwa na wajibu wa kushughulikia dhabihu nzima za kuteketezwa,^f toleo la nafaka,^g na toleo la kinywaji wakati wa sherehe,^h miezi mipya, Sabato,ⁱ na sherehe zote zilizoamriwa za nyumba ya Israeli.^j Yeye ndiye atakayetoa dhabihu ya dhambi, toleo la nafaka, dhabihu nzima ya kuteketezwa, na dhabihu za ushirika, ili kufunika dhambi za watu wa nyumba ya Israeli.’

18 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Katika mwezi wa kwanza, siku ya kwanza ya mwezi huo, unapaswa kumchukua ng’ombe dume mchanga asiye na kasoro kutoka katika mifugo, nawe utapatakasa mahali patakatifu kutokana na dhambi.^k **19** Kuhani atachukua sehemu ya damu ya dhabihu ya dhambi na kuiweka kwenye mwimo wa mlango wa hekalu,^l juu ya zile pembe nne za ukingo unaozunguka madhabahu, na juu ya mwimo wa lango la ua wa ndani. **20** Hivyo ndivyo utakavyofanya katika

45:14, 24 *Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 45

a Law 2:1

b Law 1:10

c Law 3:1

d Law 1:4
Law 6:30
Ebr 9:22

e Kut 30:14

f 1Nya 16:2
2Nya 30:24

g 1Fa 8:64

h 2Nya 35:7

i Isa 66:23

j Kum 16:16
2Nya 8:12, 13
2Nya 31:3

k Law 16:16

l Eze 41:21

Safu ya 2

a Law 4:27, 28

b Law 16:20

c Law 23:5

d Kut 12:18

e Law 4:13, 14

f Law 23:8

g Law 23:34
Kum 16:13
2Nya 7:8
Zek 14:16

SURA YA 46

h Eze 40:32

i Eze 44:1, 2

j Kut 20:9

siku ya saba ya mwezi kwa sababu ya mtu yeyote anayefanya dhambi bila kukusudia au bila kujua;^a nanyi mtatoa dhabihu ya kufunika dhambi ya hekalu.^b

21 “Katika mwezi wa kwanza, siku ya 14 ya mwezi huo, mtafanya sherehe ya Pasaka.^c Kwa siku saba mnapaswa kula mikate isiyo na chachu.^d **22** Siku hiyo kiongozi atatoa ng’ombe dume mchanga awe dhabihu ya dhambi kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wote nchini.^e **23** Kwa siku saba za sherehe atamtolea Yehova dhabihu nzima ya kuteketezwa ya ng’ombe dume saba wachanga wasio na kasoro na kondoo dume saba wasio na kasoro kila siku kwa siku hizo saba,^f atatoa pia mbuzi dume kila siku awe dhabihu ya dhambi. **24** Pia anapaswa kutoa toleo la nafaka la efa moja kwa ajili ya kila ng’ombe dume mchanga na efa moja kwa ajili ya kila kondoo dume, vilevile hini* moja ya mafuta kwa kila efa.

25 “Katika mwezi wa saba, siku ya 15 ya mwezi huo, kwa siku saba wakati wa sherehe,^g anapaswa kutoa dhabihu ileile ya dhambi, dhabihu nzima ya kuteketezwa, toleo la nafaka, na mafuta.”

46 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Lango la ua wa ndani linalotazama mashariki^h linapaswa kubaki likiwa limefungwaⁱ kwa siku sita za kazi,^j lakini siku ya Sabato na siku ya mwezi mpya linapaswa kufunguliwa. **2** Kiongozi ataingia ndani kupitia njia ya

ukumbi wa lango,^a naye atasi-mama kando ya mwimo wa lango. Makuhani watatoa dhahibu yake nzima ya kuteketezwa na dhahibu zake za ushirika, naye atainama chini kwenye kizingiti cha lango na kutoka nje. Lakini lango linapaswa kubaki wazi mpaka jioni. **3** Watu wa nchi watainama chini pia mbele za Yehova kwenye kizingiti cha lango hilo siku za Sabato na wakati wa miezi mipya.^b

4 “Siku ya Sabato kiongozi atamtolea Yehova dhahibu nzima ya kuteketezwa ya wanakondoo dume sita wasio na kasoro na kondoo dume asiye na kasoro.^c **5** Toleo la nafaka litakuwa efa moja* kwa ajili ya yule kondoo dume na chochote anachoweza kutoa kwa ajili ya wale wanakondoo dume, pamoja na hini moja* ya mafuta kwa kila efa.^d **6** Siku ya mwezi mpya atatoa ng’ombe dume mchanga wa kundi asiye na kasoro, wanakondoo sita dume, na kondoo dume mmoja; hawapaswi kuwa na kasoro.^e **7** Atatoa toleo la nafaka la efa moja kwa ajili ya yule ng’ombe dume mchanga, na efa moja kwa ajili ya yule kondoo dume, na chochote anachoweza kutoa kwa ajili ya wale wanakondoo dume. Naye anapaswa kutoa hini moja ya mafuta kwa kila efa.

8 “Kiongozi anapoingia, anapaswa kuingia kupitia njia ya ukumbi wa lango, naye anapaswa kutoka kupitia njia hiyohiyo.^f **9** Na watu wa nchi wanapoingia mbele za Yehova wakati wa sherehe,^g wale wa-

SURA YA 46

a Eze 44:3

b Zb 81:3
Isa 66:23c Hes 28:9, 10
Eze 45:17

d Eze 46:11

e Hes 28:11-15

f Eze 46:2

g Kut 23:14
Kum 16:16

Safu ya 2

a Eze 40:20

b Eze 40:24

c Eze 45:21, 24
Eze 46:6, 7

d Law 1:3

e Eze 45:17

f Eze 46:1, 2

g Kut 29:38
Hes 28:3, 5

naoingia kupitia lango la kaskazini^a ili kuabudu, wanapaswa kutoka kupitia lango la kusini,^b na wale wanaoingia kupitia lango la kusini wanapaswa kutoka kupitia lango la kaskazini. Mtu yeyote asirudi kupitia lango aliloingilia, kwa maana wanapaswa kutoa kupitia lango lililo upande mwingine. **10** Naye kiongozi aliye miongoni mwao, anapaswa kuingia wanapoingia, na kutoka wanapotoka. **11** Wakati wa sherehe na majira ya sherehe anapaswa kutoa toleo la nafaka la efa moja kwa ajili ya yule ng’ombe dume mchanga, efa moja kwa ajili ya yule kondoo dume, na chochote anachoweza kutoa kwa ajili ya wale wanakondoo dume, pamoja na hini moja ya mafuta kwa kila efa.^c

12 “Ikiwa kiongozi atatoa dhahibu nzima ya kuteketezwa^d au dhahibu za ushirika ziwe toleo la hiari kwa Yehova, atafunguliwa lango linalotazama mashariki, naye atatoa dhahibu yake nzima ya kuteketezwa na dhahibu zake za ushirika kama anavyofanya siku ya Sabato.^e Baada ya kutoa nje, lango linapaswa kufungwa.^f

13 “Kila siku unapaswa kumtoa mwanakondoo dume asiye na kasoro aliye katika mwaka wake wa kwanza awe dhahibu nzima ya kuteketeza kwa Yehova.^g Unapaswa kufanya hivyo kila asubuhi. **14** Pamoja na mwanakondoo huyo, kila asubuhi unapaswa kutoa sehemu ya sita ya efa iwe toleo la nafaka, pamoja na sehemu ya tatu ya hini ya mafuta ili inyunyizwe juu ya unga laini kama toleo la

kawaida la nafaka kwa Yehova. Hii ni sheria ya kudumu. **15** Wanapaswa kumtoa mwanakondoo dume, toleo la nafaka, na mafuta kila asubuhi kama dhabihu nzima ya kuteketezwa ya kawaida.’

16 “Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Kiongozi akimpa zawadi kila mmoja wa wanawe iwe urithi, itakuwa mali ya wanawe. Hiyo ni miliki yao waliyoriithi. **17** Lakini akimpa mmoja wa watumishi wake zawadi kutoka katika urithi wake, itakuwa yake mpaka mwaka wa uhuru;^a kisha itarudi kwa kiongozi. Urithi wa wanawe tu ndio utakaokuwa wao daima. **18** Kiongozi hapaswi kuchukua urithi wowote wa watu kwa kuwalazimisha waondoke katika mali yao. Anapaswa kuwapa wanawe urithi kutoka kwenye mali yake mwenyewe, ili mtu yeyote miongoni mwa watu wangu asiondolewe kwa lazima katika mali yake.”

19 Kisha akaniiingiza kupitia njia^b iliyokuwa kando ya lango linaloelekea kwenye vyumba vitakatifu vya kulia chakula* vya makuhani, vilivyotazama kaskazini,^c na hapo nikaona mahali upande wa nyuma kuelekea magharibi. **20** Akaniambia: “Hapa ndipo mahali ambapo makuhani watachemshia dhabihu ya hatia na dhabihu ya dhambi na mahali ambapo wataokea toleo la nafaka,^d ili wasibebe chochote na kukipeleka kwenye ua wa nje na kuwapitishia watu utakatifu.”^{*e}

46:19 *Au “vyumba vitakatifu.” **46:20** *Tnn., “kuwatakasa watu.”

SURA YA 46

a Law 25:10

b Eze 42:9

c Eze 42:1

d Law 2:4, 5

e Eze 44:19

Safu ya 2

a 2Nya 35:13

SURA YA 47

b Eze 41:2

c Zek 13:1

Zek 14:8

Ufu 22:1

d Eze 40:20

e Eze 40:6

Eze 44:1, 2

f Eze 40:3

Ufu 21:15

21 Akanitoa nje kwenye ua wa nje na kuniongoza kupitia zile pembe nne za ua, nami nikaona ua kando ya kila pembe ya ua wa nje. **22** Kwenye hizo pembe nne za ua kulikuwa na nyua ndogo, zenye urefu wa mikono 40* na upana wa mikono 30. Nyua zote nne zilikuwa na ukubwa uleule.[#] **23** Kulikuwa na vidato* kuzunguka nyua zote nne, na chini ya vidato hivyo walijenga sehemu za kuchemshia dhabihu. **24** Kisha akaniambia: “Hizi ndizo nyumba ambamo wahudumu wa hekalu huchemshia dhabihu zinazoletwa na watu.”^a

47 Kisha akanirudisha kwenye mlango wa hekalu,^b na hapo nikaona maji yakitiririka kuelekea mashariki kutoka chini ya kizingiti cha hekalu,^c kwa maana upande wa mbele wa hekalu ulitazama mashariki. Maji hayo yalikuwa yakitiririka kutoka chini upande wa kulia wa hekalu, upande wa kusini wa madhabahu.

2 Kisha akaniongoza nje kupitia lango la kaskazini^d na kunizungusha nje mpaka kwenye lango la nje linalotazama upande wa mashariki,^e nikaona maji yakitiririka kutoka upande wa kulia.

3 Mtu huyo alipotoka nje kuelekea mashariki akiwa na kamba ya kupimia mkononi mwake,^f alipima mikono 1,000* na kunipitisha katika maji; maji hayo yalifika kwenye vifundo vya miguu.

46:22; 47:3 *Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14. **46:22** #Au “Zote nne na nyua zake za pembeni zilikuwa na ukubwa uleule.” **46:23** *Au “safu.”

4 Kisha akapima mikono mingine 1,000 na kunipitisha katika maji, nayo yalifika mpaka kwenye magoti.

Akapima mikono mingine 1,000 na kunipitisha humo, na maji hayo yalifika kiunoni.

5 Alipopima mikono mingine 1,000, maji yalikuwa mengi sana hivi kwamba singeweza kuvuka, kwa maana maji hayo yalikuwa na kina kirefu hivi kwamba mtu angelazimika kuogelea, maji mengi sana ambayo mtu hangeweza kuvuka kwa miguu.

6 Akaniuliza: “Mwana wa binadamu, je, umeona hili?”

Kisha akanitembeza na kunirudisha kwenye ukingo wa kile kijito. 7 Niliporudi, nikaona miti mingi sana pande zote za ukingo wa kile kijito.^a 8 Ndipo akaniambia: “Maji haya yanatiririka kuelekea eneo la mashariki na yanashuka kupitia Araba^{*b} na kuingia baharini. Yakiingia baharini,^c maji ya bahari yataponywa. 9 Kila mahali ambapo maji hayo yanapita, makundi makubwa ya viumbe walio^{*} hai yataishi. Kutakuwa na samaki wengi, kwa sababu maji hayo yatatiririka[#] huko. Maji ya baharini yataponywa, na mahali ambapo kijito hicho kinapita, kila kitu kitaishi.

10 “Wavuvi watasimama kando yake kutoka En-gedi^d mpaka En-eglaimu ambako kutakuwa na uwanja wa ku-kaushia nyavu za kukokotwa. Kutakuwa na samaki wengi wa aina nyingi, kama samaki wa ile Bahari Kuu.^{*e}

47:8 *Au “jangwa tambarare.” 47:9 *Au “nafsi zilizo.” [#]Tnn., “vijito hivyo viwili vitatiririka.” 47:10 *Yaani, Bahari ya Mediterania.

SURA YA 47

a Ufu 22:1, 2

b Kum 4:47, 49

c Zek 14:8

d Yos 15:20, 62
2Nya 20:2

e Hes 34:2, 6

Safu ya 2

a Kum 29:22, 23
Zb 107:33, 34
Yer 17:6

b Eze 47:1

c Ufu 22:1, 2

d Mwa 48:5
1Nya 5:1
Eze 48:5e Mwa 26:3
Mwa 28:13

f Eze 48:1

g Hes 34:2, 8

h Hes 13:21

i 2Sa 8:8

j Eze 47:18

k Hes 34:2, 9

l Eze 48:1

m Hes 32:1

11 “Kutakuwa na sehemu zenye majimaji na matope, nazo hazitaponywa. Zitabaki zikiwa sehemu za chumvi.^a

12 “Aina zote za miti ya chakula zitakua kwenye kingo zote mbili za hicho kijito. Majani yake hayatanyauka; wala miti hiyo haitakosa kuzaa matunda. Kila mwezi itazaa matunda mapya, kwa sababu maji yake yanatiririka kutoka patakatifu.^b Matunda yake yatakuwa chakula na majani yake yatatumiwa kuponya.”^c

13 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: “Hili ndilo eneo ambalo mtayagawia yale makabila 12 ya Israeli kuwa urithi wao wa ardhi, na Yosefu atapata sehemu mbili.^d 14 Nanyi mtairithi na kuigawa kwa usawa.^{*} Niliapa kuwapatia mababu zenu nchi hii,^e na sasa mme-gawiwa[#] ili iwe urithi wenu.

15 “Huu ndio mpaka wa kaskazini wa nchi: Unaanzia ile Bahari Kuu kupitia njia ya Hethloni^f kuelekea Sedi,^g 16 Hamathi,^h Berotha,ⁱ na Sibraimu, kati ya eneo la Damasko na eneo la Hamathi, hadi Haser-hatikoni, karibu na mpaka wa Haurani.^j 17 Basi mpaka utaanzia baharini hadi Hasar-enoni,^k kwenye mpaka wa Damasko kuelekea kaskazini, pamoja na mpaka wa Hamathi.^l Huo ndio mpaka wa kaskazini.

18 “Upande wa mashariki mpaka huo unapita kati ya Haurani na Damasko na kando ya Yordani kati ya Gileadi^m na nchi ya Israeli. Mna-

47:14 *Tnn., “mtairithi, kila mtu kama ndugu yake.” [#]Tnn., “inawaangukia.”

paswa kupima kutoka mpakani hadi kwenye bahari ya mashariki.* Huo ndio mpaka wa mashariki.

19 "Mpaka wa kusini* utanzia Tamari hadi kwenye maji ya Meribath-kadeshi,^a kisha utaelekea kwenye lile Korongo[#] hadi kwenye ile Bahari Kuu.^b Huo ndio mpaka wa kusini.*

20 "Bahari Kuu iko upande wa magharibi, kuanzia kwenye mpaka hadi kwenye eneo lililo ng'ambo ya Lebohamathi.*^c Huo ndio mpaka wa magharibi."

21 "Mnapaswa kugawana nchi hii miongoni mwenu, miongoni mwa makabila 12 ya Israeli. **22** Mnapaswa kugawa iwe urithi miongoni mwenu wenyewe na kuwagawia wageni wanaoishi pamoja nanyi ambao wamezaa watoto wakati wanaishi miongoni mwenu; nao watakuwa kweni kama Waisraeli wenyeji. Watapokea urithi pamoja nanyi miongoni mwa makabila ya Israeli. **23** Mnapaswa kumpa mkaaji mgeni urithi katika eneo la kabila analoishi ndani yake," asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

48 "Haya ndiyo majina ya makabila hayo, kuanzia mpaka wa kaskazini: Sehemu ya Dani^d inapita kwenye njia ya Hethloni hadi Lebohamathi*^e hadi Hasar-enani, kwenye mpaka wa Damasko kuelekea kaskazini kando ya Hamathi;^f nayo inaanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka

47:18 *Yaani, Bahari ya Chumvi. **47:19** *Tnn., "upande wa kusini kuelekea kusini." [#]Yaani, Korongo la Misri. **47:20;** **48:1** *Au "njia ya kuingia Hamathi."

SURA YA 47

a Kum 32:51

b Eze 48:28

c Hes 34:2, 8

SURA YA 48

d Yos 19:40

e Hes 34:2, 8

f Eze 47:15-17

Safu ya 2

a Yos 19:24

b Yos 19:32

c Yos 13:29

d Yos 17:17, 18

e Yos 18:7

f Yos 15:1
Yos 19:9

g Eze 45:1

h Hes 35:2
Eze 45:3, 4

wa magharibi. **2** Sehemu ya Asheri^a iko kwenye mpaka wa Dani, kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **3** Sehemu ya Naftali^b iko kwenye mpaka wa Asheri, kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **4** Sehemu ya Manase^c iko kwenye mpaka wa Naftali, kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **5** Sehemu ya Efraimu iko kwenye mpaka wa Manase,^d kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **6** Sehemu ya Rubeni iko kwenye mpaka wa Efraimu,^e kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **7** Sehemu ya Yuda iko kwenye mpaka wa Rubeni,^f kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **8** Kwenye mpaka wa Yuda, kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, mchango mtakaoweka kando unapaswa kuwa na upana wa mikono 25,000,^{*g} nao unapaswa kulingana na urefu wa zile sehemu nyingine za makabila kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. Patakatifu patakuwa katikati yake.

9 "Mchango mtakaoweka kando kwa ajili ya Yehova utakuwa na urefu wa mikono 25,000 na upana wa mikono 10,000. **10** Huu ndio utakaokuwa mchango mtakatifu kwa ajili ya makuhani.^h Upande wa kaskazini utakuwa mikono 25,000, upande wa magharibi 10,000, na upande wa mashariki 10,000, na

48:8 *Hiki ni kipimo cha mikono mirefu. Angalia Nyongeza B14.

upande wa kusini 25,000. Patakatifu pa Yehova patakuwa katikati yake. **11** Patakuwa pa makuhani waliotakaswa kutoka kwa wana wa Sadoki,^a wale walioshughulikia majukumu niliyowapa na ambao hawakuniacha wakati Waisraeli na Walawi wali-poniacha.^b **12** Watapokea sehemu ya mchango wa nchi hiyo iliyowekwa kando kuwa kitu kitakatifu kabisa, kwenye mpaka wa Walawi.

13 “Kando tu ya eneo la makuhani, Walawi watakuwa na sehemu yenye urefu wa mikono 25,000, na upana wa mikono 10,000. (Urefu wote utakuwa 25,000 na upana 10,000.) **14** Hawapaswi kuuza, kubadilisha, au kumpa mtu mwingine eneo lolote la sehemu hii bora ya nchi, kwa maana ni kitu kitakatifu kwa Yehova.

15 “Eneo linalobaki lenye upana wa mikono 5,000 lililo kando ya mpaka wenye urefu wa mikono 25,000 litakuwa la matumizi ya kawaida ya jiji,^c kwa ajili ya makao na malisho. Jiji litakuwa katikati yake.^d **16** Hivi ndivyo vipimo vya jiji: Mpaka wa kaskazini mikono 4,500, mpaka wa kusini 4,500, mpaka wa mashariki 4,500, na mpaka wa magharibi 4,500. **17** Malisho ya jiji yatakuwa mikono 250 upande wa kaskazini, 250 upande wa kusini, 250 upande wa mashariki, na 250 upande wa magharibi.

18 “Urefu wa sehemu inayobaki utalingana na mchango mtakatifu,^e upande wa mashariki mikono 10,000, na upande wa magharibi 10,000. Ita-

SURA YA 48

a Eze 40:46
Eze 44:15b Yer 23:11
Eze 22:26

c Eze 45:6

d Eze 48:35

e Eze 45:1

Safu ya 2

a Eze 45:6

b Eze 45:7

c Eze 48:8

d Yos 18:11

e Yos 19:1

f Yos 19:17

g Yos 19:10

h Mwa 49:13

i Yos 18:7

lingana na mchango mtakatifu na mazao yake yatakuwa chakula cha wale wanaolitumikia jiji. **19** Wale wanaolitumikia jiji kutoka katika makabila yote ya Israeli watailima sehemu hiyo.^a

20 “Mchango mzima ni mikono 25,000 mraba. Mnapsa kuuweka kando uwe mchango mtakatifu pamoja na miliki ya jiji.

21 “Sehemu itakayobaki pande zote za mchango mtakatifu na wa miliki ya jiji itakuwa mali ya kiongozi.^b Itakuwa kando ya mipaka yenye urefu wa mikono 25,000 iliyo upande wa mashariki na magharibi wa ule mchango. Italingana na sehemu zinazopakana, na itakuwa ya kiongozi. Mchango mtakatifu na patakatifu pa hekalu patakuwa katikati yake.

22 “Miliki ya Walawi na miliki ya jiji itakuwa kati ya mali ya kiongozi. Eneo la kiongozi litakuwa kati ya mpaka wa Yuda^c na Benjamini.

23 “Na kuhusu makabila yanayobaki, sehemu ya Benjamini inaanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi.^d **24** Sehemu ya Simeoni iko kando ya mpaka wa Benjamini,^e kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **25** Sehemu ya Isakari^f iko kando ya mpaka wa Simeoni, kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi. **26** Sehemu ya Zabuloni iko kando ya mpaka wa Isakari,^g kuanzia mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi.^h **27** Sehemu ya Gadi iko kando ya mpaka wa Zabuloni,ⁱ kuanzia mpaka wa ma-

shariki hadi mpaka wa m-gharibi. **28** Mpaka wa kusini ulio kando ya mpaka wa Gadi utanzia Tamari^a hadi kwenye maji ya Meribath-kadeshi,^b hadi kwenye lile Korongo*^c na kwenda hadi kwenye ile Bahari Kuu.[#]

29 “Hii ndiyo nchi ambayo mnapaswa kuigawa iwe urithi wa makabila ya Israeli,^d na hizo ndizo zitakazokuwa sehemu zao,”^e asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

30 “Hizi ndizo zitakazokuwa njia za kutokea za jiji: Kipimo cha upande wa kaskazini kitakuwa mikono 4,500.^f

31 Malango ya jiji yatapewa majina ya makabila ya Israeli. Kati ya malango matatu ya kaskazini, kuna lango moja la

48:28 *Yaani, Korongo la Misri. #Yaani, Bahari ya Mediterania.

SURA YA 48

a Eze 47:19

b Hes 20:13

c Mwa 15:18

d Hes 34:2

e Eze 47:13

f Eze 48:16

Safu ya 2

a Yer 3:17

Yoe 3:21

Zek 2:10

Rubeni, moja la Yuda, na moja la Lawi.

32 Upande wa mashariki utakuwa na urefu wa miko-no 4,500, na malango matatu: lango moja la Yosefu, lango moja la Benjamini, na lango moja la Dani.

33 Upande wa kusini utakuwa na urefu wa mikono 4,500, nao utakuwa na malango matatu: lango moja la Simeoni, lango moja la Isakari, na lango moja la Zabuloni.

34 Upande wa magharibi utakuwa na urefu wa miko-no 4,500, nao utakuwa na malango matatu: lango moja la Gadi, lango moja la Asheri, na lango moja la Naftali.

35 “Urefu kuzunguka jiji lote utakuwa mikono 18,000. Na jina la jiji hilo kuanzia siku hiyo na kuendelea litakuwa, Yehova Yupo Hapo.”^a

DANIELI

YALIYOMO

- Yerusalemu lazingirwa na Wababiloni (1, 2)
Mafunzo maalumu ya mfalme kwa vijana waliohamishwa (3-5)
Uaminifu wa vijana wanne Waebraia wajaribiwa (6-21)
- Mfalme Nebukadneza aota ndoto ya kufadhaisha (1-4)
Wenye hekima washindwa kueleza maana ya ndoto (5-13)
Danieli amwomba Mungu msaada (14-18)
Mungu asifiwa kwa kufunua siri (19-23)
Danieli amwambia mfalme ndoto yake (24-35)
Maana ya ndoto (36-45)

- Jiwe la Ufalme laivunja sanamu (44, 45)
Danieli aheshimiwa na mfalme (46-49)
- Sanamu ya dhahabu ya Mfalme Nebukadneza (1-7)
Walazimishwa kuabudu sanamu (4-6)
Waebraia watatu washtakiwa kwa kukataa kuabudu (8-18)
“Hatutaibudu miungu yako” (18)
Watupwa kwenye tanuru la moto (19-23)
Waokolewa kimuujiza kutoka motoni (24-27)
Mfalme amsifu Mungu wa Waebraia (28-30)
 - Mfalme Nebukadneza atambua utawala wa Mungu (1-3)

- Ndoto ya mfalme kuhusu mti (4-18)
Nyakati saba kupita baada ya mti kuangushwa (16)
Mungu ni Mtawala wa wanadamu (17)
Danieli aeleza maana ya ndoto (19-27)
Utimizo wa kwanza wamhusu mfalme (28-36)
Mfalme ashikwa na wazimu kwa nyakati saba (32, 33)
Mfalme amtukuza Mungu wa mbinguni (37)
- 5 Sherehe ya mfalme Belshaza (1-4)
Maandishi ukutani (5-12)
Danieli aombwa aeleze maana ya maandishi (13-25)
Maana: Kuanguka kwa Babiloni (26-31)
- 6 Njama ya maofisa Waajemi dhidi ya Danieli (1-9)
Danieli aendelea kusali (10-15)
Danieli atupwa kwenye shimo la simba (16-24)
Mfalme Dario amheshimu Mungu wa Danieli (25-28)
- 7 Maono ya wanyama wanne (1-8)
Pembe ndogo yenye majivuno yatokea (8)
Mzee wa Siku afanya kikao (9-14)
Mwana wa binadamu apewa ufalme (13, 14)
Danieli ajulishwa maana ya maono (15-28)
Wanyama wanne ni wafalme wanne (17)
Watakatifu kupokea ufalme (18)
Kusimama kwa pembe kumi, au wafalme (24)
- 8 Maono ya kondoo na mbuzi (1-14)
Pembe ndogo yajitukuza (9-12)
Mpaka jioni na asubuhi 2,300 (14)
Gabrieli aeleza maana ya maono (15-27)
Ufafanuzi kuhusu kondoo na mbuzi (20, 21)
Kutokea kwa mfalme mkali (23-25)
- 9 Danieli atoa sala ya toba (1-19)
Miaka sabini ya ukiwa (2)
Gabrieli amtembelea Danieli (20-23)
Majuma sabini ya kinabii yatabiriwa (24-27)
Kutokea kwa Masihi baada ya majuma 69 (25)
Kuuawa kwa Masihi (26)
Kuangamizwa kwa jiji na mahali patakatifu (26)
- 10 Danieli atembelewa na mjumbe wa Mungu (1-21)
Mikaeli amsaidia malaika (13)
- 11 Wafalme wa Uajemi na Ugiriki (1-4)
Wafalme wa kusini na kaskazini (5-45)
Kutokea kwa mtozaji (20)
Kiongozi wa agano auawa (22)
Kutukuzwa kwa mungu wa ngome (38)
Mapambano kati ya mfalme wa kusini na wa kaskazini (40)
Habari za kushtua kutoka mashariki na kaskazini (44)
- 12 “Wakati wa mwisho” na baadaye (1-13)
Mikaeli atenda (1)
Wenye ufahamu watang’aa (3)
Kuenea kwa ujuzi wa kweli (4)
Danieli ataamka na kupokea fungu lake (13)

1 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Mfalme Yehoyakimu^a wa Yuda, Mfalme Nebukadneza wa Babiloni alikuja na kuzingira Yerusalemu.^b
2 Baada ya muda Yehova akamtia Mfalme Yehoyakimu wa Yuda mikononi mwake,^c pamoja na baadhi ya vyombo vya nyumba ya* Mungu wa

SURA YA 1

a 2Nya 36:4
Yer 22:18, 19
Yer 36:30

b Kum 28:49, 50
2Fa 24:1
2Nya 36:5, 6

c Isa 42:24

Safu ya 2

a Mwa 10:9, 10

b 2Nya 36:7
Ezr 1:7

kweli, akavileta katika nchi ya Shinari*^a katika nyumba ya* mungu wake. Akaviweka katika hazina ya mungu wake.^b

3 Kisha Mfalme Nebukadneza akamwagiza Ashpenazi ofisa mkuu wa makao yake ya kifalme awaleta baadhi ya Waisraeli,* kutia ndani wale wa-

1:2 *Au “hekalu la.”

1:2 *Yaani, Babilonia. 1:3 *Tnn., “wana wa Israeli.”

naotoka katika uzao wa kifalme na wa watu mashuhuri.^a **4** Walipaswa kuwa vijana* wasio na kasoro yoyote, wazuri kwa umbo, waliobarikiwa kuwa na hekima, ujuzi, na utambuzi,^b na wanaoweza kutumikia katika jumba la mfalme. Alipaswa kuwafundisha maandishi na lugha ya Wakaldayo. **5** Pia, mfalme aliagiza wapewe kila siku vyakula bora ambavyo yeye mwenyewe alikula na divai ambayo alikunywa. Walipaswa kuzoezwa* kwa miaka mitatu, na baada ya muda huo wangeanza kumtumikia mfalme.

6 Sasa baadhi ya vijana hao walikuwa wa kabila la* Yuda: Danieli,^c Hanania,^d Mishaeli,^e na Azaria.^f **7** Na ofisa mkuu wa makao ya mfalme akawapa majina;* alimpa Danieli jina Belteshaza,* akampa Hanania jina Shadraki, akampa Mishaeli jina Meshaki, na kumpa Azaria jina Abednego.^f

8 Lakini Danieli aliazimia moyoni mwake kwamba hatajichafua kwa vyakula bora vya mfalme wala divai yake. Basi akamwomba ofisa mkuu wa makao ya mfalme ruhusa ya kutojichafua kwa njia hiyo. **9** Na Mungu wa kweli akamfanya ofisa mkuu wa makao ya mfalme amtendee Danieli kwa fadhili* na rehema.^g

1:4, 10, 13, 15, 17 *Tnn., "watoto." 1:5 *Au labda, "kulishwa." 1:6 *Tnn., "wana wa." #Maana yake "Mwamuzi Wangu Ni Mungu." ^Maana yake "Yehova Ameonyesha Kibali." @Huenda jina hili linamaanisha "Ni Nani Aliye Kama Mungu?" □Maana yake "Yehova Amesaidia." 1:7 *Yaani, majina ya Kibabiloni. 1:9 *Tnn., "amwonyeshe Danieli kibali."

SURA YA 1

a 2Fa 20:16, 18

b Da 1:17, 20
Da 5:11, 12c Da 2:48
Da 5:13, 29

d Da 2:17, 18

e Da 4:8
Da 5:12f Da 2:49
Da 3:12, 28g 1Fa 8:49, 50
Zb 106:44, 46

Safu ya 2

a Da 1:20
Da 4:9
Da 5:11, 12

b Da 1:5

10 Lakini ofisa mkuu wa makao ya mfalme akamwambia Danieli: "Ninamwogopa bwana wangu mfalme, ambaye ametoa maagizo kuhusu vyakula na vinywaji vyeenu. Itakuwaje akiona kwamba afya yenu ni mbaya kuliko ya vijana* wengine wa rika lenu? Mtanifanya niwe na[#] hatia mbele ya mfalme." **11** Lakini Danieli akamwambia mtu aliyeteuliwa na ofisa mkuu wa makao ya mfalme ili kumtunza yeye, Hanania, Mishaeli, na Azaria: **12** "Tafadhali, tujaribu sisi watumishi wako kwa siku kumi, tupe mboga za majani na maji ya kunywa; **13** kisha linganisha sura zetu na sura za vijana* wanaokula vyakula bora vya mfalme, halafu ututendee sisi watumishi wako kulingana na jinsi tunavyoonekana machoni paka."

14 Basi akakubali pendekizo lao na kuwajaribu kwa siku kumi. **15** Baada ya siku kumi sura yao ilikuwa nzuri zaidi na yenye afya zaidi* kuliko ya vijana* wote waliokuwa wakila vyakula bora vya mfalme. **16** Kwa hiyo mtu aliye-watunza alikuwa akichukua vyakula vyao bora na divai yao na kuwapa mboga za majani. **17** Na Mungu wa kweli aliwapa vijana* hao wanne ujuzi na ufahamu wa kila aina ya maandishi na hekima; naye Danieli alipewa uwezo wa kuelewa maono na ndoto za kila aina.^a

18 Mwishoni mwa kipindi ambacho mfalme aliagiza vijana wote waletwe ndani,^b ofisa mkuu wa makao

1:10 #Tnn., "Mtakifanya kichwa changu kiwe na." 1:15 #Tnn., "miili yao ilinepepa."

ya mfalme aliwaleta mbele ya Nebukadneza. **19** Mfalme alipozungumza nao, hakuna kijana yeyote katika kikundi chote aliyekuwa kama Danieli, Hanania, Mishaeli, na Azaria;^a nao wakaendelea kumtumikia mfalme. **20** Katika kila jambo lililohitaji hekima na uelewaji ambalo mfalme aliwauliza, aliona kwamba walikuwa bora mara kumi kuliko makuhani wote wachawi na watu waliofanya mazingaombwe^b katika milki yake yote. **21** Danieli alibaki huko mpaaka mwaka wa kwanza wa Mfalme Koreshi.^c

2 Katika mwaka wa pili wa utawala wake, Nebukadneza aliota ndoto kadhaa, akahangaika* sana^d hivi kwamba akashindwa kulala. **2** Basi mfalme akaagiza makuhani wachawi, watu wanaofanya mazingaombwe, walozi, na Wakaldayo* waitwe ili wawambie mfalme ndoto zake. Kwa hiyo wakaja na kusimama mbele ya mfalme.^e **3** Kisha mfalme akawaambia: “Nimeota ndoto, nami ninahangaika* kwa sababu ninataka kujua nilichoota.” **4** Wakaldayo wakamjibu mfalme kwa lugha ya Kiaramu:^{*f} “Ee mfalme, na uishi milele. Tusimulie ndoto yako sisi watumishi wako, nasi tutakuambia maana yake.”

5 Mfalme akawajibu Wakaldayo: “Nimeamua hivi: Msiponiambia ndoto yangu na kunieleza maana yake, mtaka-

2:1 *Tnn., “roho yake ikahangaika.” 2:2 *Yaani, kikundi kilichokuwa stadi katika ubashiri na unajimu. 2:3 *Tnn., “roho yangu inahangaika.” 2:4 *Sehemu ya Da 2:4b hadi 7:28 iliandikwa kwa Kiaramu.

SURA YA 1

a Da 1:3, 6

b Da 2:2
Da 4:7
Da 5:8c Da 6:28
Da 10:1

SURA YA 2

d Da 4:4, 5

e Da 4:6, 7
Da 5:7, 8f 2Fa 18:26
Ezr 4:7
Isa 36:11

Safu ya 2

a Da 2:48
Da 5:16, 29

b Da 2:24

twaw vipandevipande, na nyumba zenu zitageuzwa kuwa vyoo vya umma.* **6** Lakini mkiniambia ndoto yangu na kunieleza maana yake, nita-wapa zawadi na tuzo na heshima kubwa.^a Basi niambi- ni ndoto hiyo na maana yake.”

7 Wakamjibu kwa mara ya pili: “Ee mfalme, tuambie ndoto yako, sisi watumishi wako, nasi tutakueleza maana yake.”

8 Mfalme akawajibu: “Najua vema kwamba mnajaribu kujipatia muda, kwa kuwa mnajua uamuzi wangu. **9** Msiponiambia ndoto yangu, adhabu yenu nyote ni moja tu. Lakini mmekubaliana kunidangan- nya na kunihadaa, mkitumaini kwamba hali itabadilika. Basi niambi- ni ndoto hiyo, nami nitajua kwamba mnaweza kueleza maana yake.”

10 Wakaldayo wakamjibu mfalme: “Hakuna mtu yeyote duniani* anayeweza kufanya jambo ambalo wewe mfalme unaagiza, kwa sababu hakuna mfalme yeyote mkuu wala gavana aliyewahi ku- mwomba kuhani yeyote mchawi, au mtu yeyote anayefanya mazingaombwe, au Mkaldayo afanye jambo kama hili. **11** Jambo ambalo wewe mfalme unaomba ni gumu, na hakuna yeyote anayeweza kukwambia jambo hilo isipoku- wa miungu, ambao hawaishi miongoni mwa wanadamu.”*

12 Ndipo mfalme akashikwa na ghadhabu kali, akaagiza wanaume wote wenye hekima wa Babiloni waangamizwe.^b

2:5 *Au labda, “maeneo ya takataka; marundo ya mavi.” 2:10 *Au “katika nchi kavu.” 2:11 *Tnn., “wenye mwili wa nyama.”

13 Agizo hilo lilipotolewa na wakati ulipokaribia wa kuwaua wanaume hao wenye hekima, walimtafuta pia Danieli na wenzake ili wawaue.

14 Wakati huo, kwa busara na tahadhari Danieli alizungumza na Arioko mkuu wa walinzi wa mfalme, alipokuwa akienda kuwaua wanaume wenye hekima wa Babiloni.

15 Akamuuliza Arioko ofisa wa mfalme: “Kwa nini mfalme ametoa agizo kali hivyo?” Ndi-po Arioko akamweleza Danieli jambo hilo.^a **16** Basi Danieli akaenda na kumwomba mfalme ampe muda ili amweleze maana ya ndoto yake.

17 Kisha Danieli akarudi nyumbani kwake na kuwajulisha wenzake, Hanania, Mishaeli, na Azaria kuhusu jambo hilo. **18** Akawaambia wasali ili Mungu wa mbinguni awaonyeshe rehema na kuwajulisha siri hiyo, ili yeye Danieli, na wenzake wasiangamizwe pamoja na wale wanaume wengine wenye hekima wa Babiloni.

19 Kisha Danieli akafunuliwa siri hiyo katika maono wakati wa usiku.^b Basi Danieli akamsifu Mungu wa mbinguni. **20** Danieli akasema:

“Jina la Mungu na lisifiwe kwa umilele wote,^{*}
Kwa maana hekima na uwezo ni wake peke yake.^c”

21 Yeye hubadili nyakati na majira,^d

Huwaondoa wafalme na kuwaweka wafalme,^e

Huwapa hekima walio na hekima na kuwapa ujuzi wale walio na utambuzi.^f

SURA YA 2

a Da 2:9

b Da 2:28

c 1Nya 29:11
Ayu 12:13
Zb 147:5
Yer 32:17-19

d Mdo 1:7

e 1Sa 2:7, 8
Zb 75:7
Yer 27:5
Da 4:17

f Met 2:6
Mhu 2:26
Yak 1:5

Safu ya 2

a Yer 33:3
1Ko 2:10

b Zb 139:12
Ebr 4:13

c Zb 36:9
Zb 112:4

d Da 1:17
Da 2:28

e Da 2:12, 14

f Da 1:3, 6

g Da 1:7

h Mwa 41:15

i Da 2:10, 11

j Mwa 40:8
Da 1:17

22 Yeye hufunua mambo yenye kina na mambo yali-yofichika,^a
Anajua yaliyo gizani,^b
Na nuru hukaa pamoja naye.^c

23 Ee Mungu wa mababu zangu, ninakushukuru na kukusifu,

Kwa sababu umenipa hekima na nguvu.

Na sasa umenijulisha tulichokuomba;

Umetujulisha jambo linalomhangaisha mfalme.^d

24 Kisha Danieli akaenda kwa Arioko, ambaye alikuwa ameteuliwa na mfalme kuwaangamiza wanaume wenye hekima wa Babiloni,^e akamwambia: “Usimwagamize mwanamume yeyote mwenye hekima wa Babiloni. Nipeleke mbele ya mfalme, nami nita-mweleza mfalme maana ya ndoto yake.”

25 Mara moja Arioko akampeleka Danieli mbele ya mfalme na kumwambia: “Nimempata mwanamume fulani miongoni mwa watu waliohamishwa kutoka Yuda^f anayeweza kukueleza maana ya ndoto yako.” **26** Mfalme akamuuliza Danieli, aliyeitwa Belteshaza:^g “Je, kweli unaweza kuniambia ndoto niliyoota, na maana yake?”^h

27 Danieli akamjibu mfalme: “Hakuna mwanamume yeyote mwenye hekima, wala mtu anayefanya mazingaombwe, wala kuhani yeyote mchawi, wala mnajimu yeyote anayeweza kukufunulia wewe mfalme siri unayoomba ifunuliwe.ⁱ **28** Lakini kuna Mungu mbinguni ambaye ni Mfunuaji wa siri,^j naye amekujulisha wewe Mfalme

Nebukadneza mambo yatakayotukia katika kipindi cha mwisho cha zile siku. Hii ndiyo ndoto yako, na haya ndiyo maono yaliyokujia kichwani ulipokuwa umelala kitandani:

29 “Ee mfalme, ulipokuwa kitandani uliona katika mawazo yako mambo yatakayotukia wakati ujao, na Mfunuaji wa siri amekujulisha mambo yatakayotukia. **30** Lakini siri hii imefunuliwa kwangu si kwa sababu nina hekima nyingi zaidi kuliko mtu yeyote anayeishi, bali ilifunuliwa kwangu ili nikueleze wewe mfalme maana ya ndoto yako ili ujue mawazo yaliyo moyoni mwako.^a

31 “Wewe, Ee mfalme, ulitazama na kuona sanamu kubwa sana. Sanamu hiyo, iliyo kuwa kubwa sana na iliyong’aa kupita kiasi, ilisimama mbele yako, nayo ilikuwa yenye kutisha. **32** Kichwa cha sanamu hiyo kilikuwa cha dhahabu bora,^b kifua chake na mikono yake ilikuwa ya fedha,^c tumbo na mapaja yake yalikuwa ya shaba,^d **33** miguu yake ilikuwa ya chuma,^e na kwa sehemu, nyayo zake zilikuwa za chuma na kwa sehemu zilikuwa za udongo wa mfinyanzi.*^f **34** Uliendelea kutazama hadi jiwe likakatwa, si kwa mikono, nalo likaipiga sanamu hiyo kwenye nyayo zake za chuma na za udongo wa mfinyanzi na kuzipondaponda.^g **35** Wakati huo kile chuma, ule udongo wa mfinyanzi, ile shaba, ile fedha, na ile dhahabu, vyote pamoja, vikapondwapondwa na kuwa kama makapi kuto-

2:33 *Au “udongo wa mfinyanzi (uliofiinyangwa) uliochomwa.”

SURA YA 2

a Da 2:47

b Da 2:37,38

Da 7:4

c Da 5:28

Da 7:5

Da 8:3, 20

d Da 2:39

Da 7:6

Da 8:5, 21

e Da 7:7, 19

f Da 2:40-42

g Da 2:44, 45

Safu ya 2

a Yer 28:14

Da 5:18

b Yer 27:5-7

c Da 2:32

Da 4:20-22

d Isa 45:1

Yer 51:28, 29

Da 5:28

e Da 7:6

Da 8:5, 21

Da 11:3

f Da 2:33

Da 7:19, 23

g Da 7:7

ka kwenye uwanja wa kupuria wakati wa kiangazi, kisha upepo ukavipeperusha mbali hivi kwamba hakuna chembe yoyote ya vitu hivyo ingeweza kupatikana. Lakini lile jiwe lili loipiga ile sanamu likawa mlina mkubwa, nalo likaijaza dunia yote.

36 “Hiyo ndiyo ndoto yako, na sasa tutakueleza maana yake. **37** Wewe, Ee mfalme —mfalme wa wafalme ambaye Mungu wa mbinguni amekupa ufalme,^a uwezo, nguvu, na utukufu, **38** na kuwaweka mikononi mwako wanadamu mahali popote ambapo hue nda wanaishi, na pia wanyama wa mwituni na ndege wa angani, na kukufanya kuwa mtawala juu ya hao wote^b—wewe mwenyewe ndiye kichwa cha dhahabu.^c

39 “Lakini baada yako ufalme mwingine utainuka,^d ulio dhaifu kwako; kisha ufalme mwingine, wa tatu, wa shaba, ambao utaitawala dunia yote.^e

40 “Ufalme wa nne utakuwa wenye nguvu kama chuma.^f Kwa maana kama vile chuma kinavyopondaponda na kusagasaga vitu vingine vyote, naam, kama chuma kinachovunjavunja, ufalme huo utapondaponda na kuzivunjavunja falme hizo zote.^g

41 “Na kama tu ulivyoona kwamba nyayo na vidole vya miguu kwa sehemu vilikuwa vya udongo wa mfinyanzi na kwa sehemu vilikuwa vya chuma, ufalme huo utagawanyika, lakini ugumu fulani wa chuma utakuwa ndani yake, kama tu ulivyoona chuma kikiwa kimechanganyika na udongo laini wa mfinyanzi.

42 Na kama vile vidole vyake vya miguu vilikuwa kwa sehemu vya chuma na kwa sehemu vya udongo wa mfinyanzi, ndivyo ufalme huo utakavyokuwa na nguvu kwa sehemu na kuwa dhaifu kwa sehemu.

43 Kama tu ulivyoona chuma kikiwa kimechanganyika na udongo laini wa mfinyanzi, sehemu hizo zitachanganyika na wanadamu;* lakini hazitashikamana na wanadamu, kama tu chuma kisivyochanganyika na udongo wa mfinyanzi.

44 "Katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme^a ambao hautaangamizwa kamwe.^b Na watu wengine hawatakabidhiwa ufalme huo.^c Utazipondaponda na kuzikomesha falme hizi zote,^d nao pekee utasimama milele.^e **45** kama tu ulivyoona kwamba jiwe ambalo halikukatwa kwa mikono lilitoka kwenye mlima, na kwamba lilipondaponda kile chuma, ile shaba, ule udongo wa mfinyanzi, ile fedha, na ile dhahabu.^f Mungu Mtukufu amemjulisha mfalme mambo yatakayotukia wakati ujao.^g Ndoto hiyo ni ya kweli, na maana yake inategemeka."

46 Ndipo Mfalme Nebukadnezar akaanguka chini kifu-difudi mbele ya Danieli na kumpa heshima kubwa. Naye akaagiza apewe zawadi na kufukiziwa uvumba. **47** Mfalme akamwambia Danieli: "Kwa kweli Mungu wako ni Mungu wa miungu na Bwana wa wafalme na Mfunuaji wa siri, kwa sababu uliweza kufunua siri hii."^h **48** Kisha mfal-

2:43 *Au "uzao wa wanadamu," yaani, watu wa kawaida.

SURA YA 2

a Mwa 49:10
Zb 2:6
Mt 6:10
Lu 22:29
Yoh 18:36
Ufu 11:15
Ufu 20:6

b 2Sa 7:13
Isa 9:7
Da 7:13, 14

c Da 4:17
Da 7:27

d Zb 2:7-9
Zb 110:5, 6
Ufu 19:15

e Da 4:34
Lu 1:31-33

f Da 2:34, 35

g Mwa 41:28
Da 2:28

h Mwa 41:39
Da 1:17
Da 2:28
Da 4:9

Safu ya 2

a Da 2:6
Da 5:16, 29

b Da 1:7

me akampandisha cheo Danieli na kumpa zawadi nyingi bora, naye akamfanya kuwa mtawala wa mkoa wote wa* Babiloni^a na msimamizi mkuu wa wanaume wote wenye hekima wa Babiloni. **49** Na kwa ombi la Danieli, mfalme akawaweka Shadraki, Meshaki, na Abednego^b kuwa wakuu wa usimamizi wa mkoa wa* Babiloni, lakini Danieli alifanya kazi katika makao ya mfalme.

3 Mfalme Nebukadnezar alitengeneza sanamu ya dhahabu yenye urefu wa mikono 60[#] na upana wa mikono 6.[^] Akaisimamisha kwenye nchi tambarare ya Dura katika mkoa wa* Babiloni. **2** Kisha Mfalme Nebukadnezar akatuma ujumbe ili kuwakusanya maliwali, wasimamizi, magavana, washauri, watunza-hazina, waamuzi, mahakimu, na wasimamizi wote wa mikoa* waje kwenye sherehe ya kuzindua sanamu ambayo Mfalme Nebukadnezar alikuwa amesimamisha.

3 Basi maliwali, wasimamizi, magavana, washauri, watunza-hazina, waamuzi, mahakimu, na wakuu wote wa mikoa* wakakusanyika kwa ajili ya sherehe ya kuzindua sanamu ambayo Mfalme Nebukadnezar alikuwa amesimamisha. Nao wakasimamisha mbele ya sanamu iliyo-simamishwa na Nebukadnezar. **4** Mpiga mbiu akatanga-za hivi kwa sauti kubwa: "Enyi watu wa makabila, mataifa, na

2:48 *Au "wilaya yote ya utawala ya." 2:49; 3:1 *Au "wilaya ya utawala ya." 3:1 #Mita 27 hivi (futi 88). Angalia Nyongeza B14. ^Mita 2.7 hivi (futi 8.8). Angalia Nyongeza B14. 3:2, 3 *Au "wilaya za utawala."

lugha zote, mnaamriwa kwamba, **5** wakati mtakaposikia sauti ya pembe, zumari, zeze, kinubi cha pembe tatu, kinanda, zumari-tete, na ala nyingine zote za muziki, lazima mwanguke chini na kuabudu sanamu ya dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza amesimamisha. **6** Yeyote ambaye hataanguka chini na kuabudu atatupwa mara moja katika tanuru lenye moto mkali.^a **7** Basi watu wote waliposikia sauti ya pembe, zumari, zeze, kinubi cha pembe tatu, kinanda, zumari-tete, na ala nyingine zote za muziki, watu wa makabila, mataifa, na lugha zote wakaanguka chini na kuiabudu sanamu ya dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza alikuwa amesimamisha.

8 Wakati huo Wakaldayo fulani wakajitokeza na kuwashtaki* Wayahudi. **9** Wakamwambia Mfalme Nebukadneza: “Ee mfalme, na uishi milele. **10** Wewe, Ee mfalme, ulitoa amri kwamba kila mtu anayesikia sauti ya pembe, zumari, zeze, kinubi cha pembe tatu, kinanda, zumari-tete, na ala nyingine zote za muziki, anapaswa kuanguka chini na kuiabudu ile sanamu ya dhahabu; **11** na kwamba yeyote ambaye hataanguka chini na kuiabudu anapaswa kutupwa katika tanuru lenye moto mkali.^b **12** Lakini kuna Wayahudi fulani uliowaweka kuwa wasimamizi wa mkoa wa* Babiloni: Shadraki, Meshaki, na Abednego.^c Wanaume hawa hawajakuheshimu wewe, Ee mfalme. Ha-

3:8 *Au “kuwachongea.” 3:12 *Au “wila ya utawala ya.”

SURA YA 3

a Yer 29:22

b Da 3:4-6

c Da 1:7
Da 2:49

Safu ya 2

a Isa 46:1
Yer 50:2
Da 2:47

b Kut 5:2
2Nya 32:15
Isa 36:4, 20

c 1Sa 17:37
Zb 27:1
Isa 12:2
Da 6:27

d Kut 20:5
Mdo 5:29

waabudu miungu yako, na wanakataa kuabudu sanamu ya dhahabu ambayo umesimamisha.”

13 Ndipo Nebukadneza, kwa hasira kali sana, akaagiza Shadraki, Meshaki, na Abednego waletwe mbele yake. Basi wanaume hao wakaletwa mbele ya mfalme. **14** Nebukadneza akawauliza: “Shadraki, Meshaki, na Abednego, je, ni kweli kabisa kwamba hamwabudu miungu yangu^a na kwamba mnakataa kuabudu sanamu ya dhahabu ambayo nimesimamisha? **15** Basi mtakaposikia sauti ya pembe, zumari, zeze, kinubi cha pembe tatu, kinanda, zumari-tete, na ala nyingine zote za muziki, mkiwa tayari kuanguka chini na kuabudu sanamu ambayo nimeitengeneza, ni sawa. Lakini mkikataa kuabudu, mtatupwa mara moja katika tanuru lenye moto mkali. Na ni mungu gani anayeweza kuwaokoa kutoka mikononi mwangu?”^b

16 Shadraki, Meshaki, na Abednego wakamjibu mfalme: “Ee Nebukadneza, hatuhitaji kukujibu kuhusiana na jambo hili. **17** Ikiwa ni lazima iwe hivyo, Mungu wetu tunayemtumikia anaweza kutuokoa kutoka katika tanuru hilo lenye moto mkali, Ee mfalme, na kutuokoa kutoka mikononi mwako.^c **18** Lakini hata asipotuoakoa, Ee mfalme, ujue kwamba hatutaabudu miungu yako wala kuabudu sanamu ya dhahabu uliyosimamisha.”^d

19 Ndipo Nebukadneza akawakasirikia vikali Shadraki, Meshaki, na Abednego hivi kwamba sura yake ika-

badilika* kuwaelekea, aka-giza tanuru liongezwe moto mara saba kuliko kawaida. **20** Akawaagiza wanaume fulani hodari katika jeshi lake wawafunge Shadraki, Meshaki, na Abednego na kuwatupa katika tanuru hilo lenye moto mkali.

21 Basi wanaume hao wakafungwa wakiwa na majoho yao, mavazi, kofia, na nguo zao nyingine, nao wakatupwa katika tanuru hilo lenye moto mkali. **22** Kwa sababu amri ya mfalme ilikuwa kali sana na tanuru lilikuwa na moto mkali isivyo kawaida, miali ya moto huo iliwaua wanaume waliowapeleka Shadraki, Meshaki, na Abednego. **23** Lakini wanaume hao watatu, Shadraki, Meshaki, na Abednego, wakaanguka ndani ya tanuru hilo lenye moto mkali wakiwa wamefungwa.

24 Ndipo Mfalme Nebukadneza akaogopa, akainuka haraka na kuwauliza maofisa wake wakuu: "Je, hatukuwafunga wanaume watatu na kuwatupa ndani ya moto?" Wakamjibu mfalme: "Naam, Ee mfalme." **25** Mfalme akasema: "Tazama! Naona wanaume wanne wakitembeatembea katikati ya moto wakiwa huru, nao hawajapatwa na madhara, na yule wa nne anaonekana kama mwana wa miungu."

26 Nebukadneza akaukaribia mlango wa lile tanuru lenye moto mkali na kusema: "Shadraki, Meshaki, na Abednego, ninyi watumishi wa Mungu Aliye Juu Zaidi,^a tokeni nje, mje hapa!" Sha-

3:19 *Au "mtazamo wake ukabadilika kabisa."

SURA YA 3

a Da 2:47

Safu ya 2

a Da 3:2

b Ebr 11:33, 34

c Da 2:47
Da 4:34

d Da 3:15

e Da 4:35
Da 6:26, 27

f Da 2:49

draki, Meshaki, na Abednego wakatoka katikati ya moto. **27** Na maliwali, wasimamizi, magavana, na maofisa wakuu wa mfalme waliokuwa wamekusanyika mahali hapo^a wakaona kwamba moto haukuwadhuru* wanaume hao;^b hakuna unywele hata mmoja wa vichwa vyao uliokuwa umeungua, majoho yao hayakuwa yamebadilika, na miili yao haikuwa hata na harufu ya moto.

28 Ndipo Nebukadneza akatangaza hivi: "Na asifiwe Mungu wa Shadraki, Meshaki, na Abednego,^c aliyemtuma malai-ka wake na kuwaokoa watumishi wake. Walimtegemea yeye na kutenda kinyume cha amri ya mfalme na walikuwa tayari kufa* badala ya kumtumikia au kumwabudu mungu mwingine yeyote isipokuwa Mungu wao wenyewe.^d **29** Kwa hiyo ninaagiza kwamba watu wa kabila lolote, taifa, au lugha ambao watasema jambo lolote dhidi ya Mungu wa Shadraki, Meshaki, na Abednego, wanapaswa kukatwa vipandevipande, na nyumba zao zinapaswa kugeuzwa kuwa vyoo vya umma;^e kwa maana hakuna mungu mwingine yeyote anayeweza kuokoa kama huyu."^e

30 Kisha mfalme akawapandisha vyeo* Shadraki, Meshaki, na Abednego katika mkoa wa^f Babiloni.^f

4 "Mimi Mfalme Nebukadneza, nawaandikia watu wa makabila yote, mataifa, na lugha zote duniani: Amani yenu

3:27 *Au "haukuwazidi nguvu." 3:28 *Au "na kutoa miili yao." 3:29 *Au labda, "maeneo ya takataka; marundo ya mavi." 3:30 *Tnn., "akawafanikisha." *Au "wilaya ya utawala ya."

na iongezeke! **2** Ninafurahi kuwatangazia ishara na maajabu ambayo Mungu Aliye Juu Zaidi amenifanyia. **3** Jinsi ishara zake zilivyo kuu, na jinsi maajabu yake yalivyo yene-nye nguvu! Ufalme wake ni ufalme wa milele, na utawala wake unadumu kizazi hata kizazi.^a

4 "Mimi, Nebukadneza, nilikuwa nikistarehe nyumbani mwangu na kufurahia ufanisi katika jumba langu la kifalme. **5** Niliota ndoto iliyoniogopesha. Nilipokuwa nimelala kitandani mwangu, njozi na maono ya kichwa changu yalinitisha.^b **6** Basi nikaagiza wanaume wote wenye hekima wa Babiloni waletwe mbele yangu ili wanieleze maana ya ndoto hiyo.^c

7 "Wakati huo makuhani wachawi, watu wanaofanya mazingaombwe, Wakaldayo,* na wanajimu^d wakaja mbele yangu. Nilipowasimulia ndoto hiyo, walishindwa kuni-eleza maana yake.^e **8** Mwishowe Danieli akaja mbele yangu, anayeitwa pia Belteshaza,^f jina la mungu wangu,^g na ambaye ana roho ya miungu mitakatifu,^h nami nikamwambia ndoto hiyo:

9 "Ee Belteshaza mkuu wa makuhani wachawi,ⁱ ninajua vema kwamba roho ya miungu mitakatifu imo ndani yako,^j na hakuna siri yoyote iliyo ngumu sana kwako.^k Basi nieleze maono niliyoona katika ndoto yangu na maana yake.

10 "Katika maono ya kichwa changu nilipokuwa kitandani mwangu, niliona mti/

4:7 *Yaani, wabashiri na wanajimu hodari.

SURA YA 4

a Zb 10:16
Zb 90:2
Yer 10:10

b Da 2:1

c Da 2:2

d Isa 47:13

e Da 2:10, 11

f Da 1:7

g Isa 46:1
Yer 50:2

h Da 4:18
Da 5:11, 12

i Da 1:20
Da 2:48

j Mwa 41:38
Da 6:3

k Da 1:17, 20

l Da 4:26

Safu ya 2

a Da 4:20-22

b Da 4:23-26

c Da 4:31
Da 5:18, 20

d Da 4:32, 33

e Lu 21:24

f Da 4:32

g Da 4:13

h Da 4:34

katikati ya dunia, nao ulikuwa mrefu kwelikweli.^a **11** Mti huo ulikua na kuimarika, na kilele chake kikafika mbinguni, nao ulionekana hadi kwenye miisho ya dunia nzima. **12** Majani yake yalipendeza, na matunda yake yalikuwa mengi, nao ulikuwa na chakula kwa ajili ya wote. Wanyama wa mwituni walitafuta kivilu chini yake, na ndege wa angani walikaa kwenye matawi yake, na viumbe wote* walipata chakula kutoka katika mti huo.

13 "Nilipokuwa nikitazama maono ya kichwa changu nikiwa kitandani mwangu, nilimwona mlinzi, mtakatifu, aki-shuka kutoka mbinguni.^b

14 Akasema hivi kwa sauti kubwa: "Ukateni na kuuangusha mti huu,^c yakateni matawi yake, yapukutisheni majani yake, na kutawanya matunda yake! Wanyama na wakimbie kutoka chini yake, na ndege kutoka kwenye matawi yake.

15 Lakini kiacheni kisiki na majizi yake ardhini kati ya majani ya shambani, kikiwa na pingo ya chuma na ya shaba. Acheni umande wa mbinguni ukiloweshe, na acheni fungu lake liwe pamoja na wanyama, kati ya majani ya dunia.^d

16 Moyo wake na ubadilishwe usiwe wa mwanadamu, nacho kipewe moyo wa mnyama, na acheni nyakati saba^e zipite.^f

17 Hilo ni kwa agizo la walinzi,^g na ombi hilo ni kwa neno la watakatifu, ili watu walio hai wajue kwamba Aliye Juu Zaidi ni Mtawala katika ufalme wa wanadamu^h na kwamba yeye humpa ufalme huo yeyo-

4:12 *Tnn., "wote wenye mwili."

te anayetaka kumpa, naye hmweka juu ya ufalme huo hata mwanadamu wa hali ya chini zaidi.”

18 “Hiyo ndiyo ndoto ambayo mimi, Mfalme Nebukadneza, niliota; sasa, Ee Belteshaza, nieleze maana ya ndoto hiyo, kwa maana wanaume wengine wote wenye hekima katika ufalme wangu wameshindwa kunieleza maana yake.^a Lakini wewe unaweza kufanya hivyo, kwa sababu roho ya miungu mitakatifu imo ndani yako.’

19 “Wakati huo Danieli, anayetwa Belteshaza, akaduwaa kwa muda, na mawazo yake yakaanza kumtisha.

“Mfalme akasema, ‘Ee Belteshaza,^b usiruhusu ndoto hii na maana yake ikutishe.’

“Belteshaza akamwambia, ‘Ee bwana wangu, ndoto hii na iwahusu wale wanaokuchukia, na maana ya ndoto hiyo itimie kwa maadui wako.

20 “Mti ulioona ambao ulikua mpaka ukawa mkubwa na kuimarika, ambao kilele chake kilifika mbinguni na ambao ulionekana duniani pote,^c **21** uliokuwa na majani yanayopendeza, matunda mengi, na chakula kwa ajili ya wote, na ambao chini yake wanyama wa mwituni waliishi na ndege wa angani kukaa kwenye matawi yake,^d **22** ni wewe, Ee mfalme, kwa sababu umekuwa mkuu na umeimarika, na utukufu wako umeongezeka na kufika mbinguni,^e na utawala wako kwenye miisho ya dunia.^f

23 “Wewe mfalme ulimwona mlinzi, mtakatifu,^g akishuka kutoka mbinguni, aliyekuwa akisema: “Ukateni na ku-

SURA YA 4

a Isa 47:13
Da 2:27
Da 5:8, 15

b Da 1:7

c Da 4:10, 11

d Da 4:12

e Isa 14:13, 14

f Da 2:37, 38

g Da 4:13
Da 8:13

Safu ya 2

a Da 4:13-16
Lu 21:24

b Da 4:31-33

c Lu 21:24
Ufu 12:6, 14

d Da 4:16

e 1Sa 2:7, 8
Ayu 34:24
Yer 27:5
Eze 21:26, 27
Da 2:21
Da 7:13, 14
Lu 1:32, 33

f Da 4:15

g 1Fa 21:29
Yoe 2:14
Yon 3:8-10

uangusha chini mti huu na kuuharibu, lakini kiacheni kisiki na mizizi yake ardhini ki-kiwa na pingu ya chuma na ya shaba, katikati ya majani ya shambani. Na acheni umande wa mbinguni ukiloweshe, na acheni fungu lake liwe pamoja na wanyama wa mwituni mpaka nyakati saba zipite.”^a **24** Ee mfalme, hii ndiyo maana yake; ni agizo la Aliye Juu Zaidi ambalo lazima litimie kwako bwana wangu mfalme. **25** Utafukuzwa mbali kutoka miongoni mwa wanadamu, utaishi na wanyama wa mwituni, nawe utapewa majani ule kama ng’ombe dume; na utalowa kwa umande wa mbinguni,^b na nyakati saba^c zitapita,^d mpaka utakapojua kwamba Aliye Juu Zaidi ni Mtawala katika ufalme wa wanadamu na kwamba yeye humpa ufalme huo yeyote anayetaka kumpa.^e

26 “Lakini kwa sababu walisema kisiki cha mti huo kiachwe pamoja na mizizi yake,^f utarudishiwa tena ufalme wako baada ya kujua kwamba mbingu zinatawala. **27** Kwa hiyo, Ee mfalme, shauri langu na likubalike kwako. Geuka uziache dhambi zako kwa kutenda yaliyo sawa, na uache uovu wako kwa kuwaonyesha maskini rehema. Huenda muda wa ufanisi wako ukarefushwa.”^g

28 Hayo yote yalimpata Mfalme Nebukadneza.

29 Miezi kumi na miwili baadaye alikuwa akitembea kwenye paa la jumba lake la kifalme la Babiloni. **30** Mfalme alikuwa akisema: “Je, hii si Babiloni Kubwa ambayo

nimeijenga mimi mwenyewe kuwa makao ya kifalme kwa nguvu zangu mwenyewe na uwezo wangu na kwa ajili ya utukufu wa ukuu wangu?"

31 Mfalme alipokuwa akieledelea kusema maneno hayo, sauti ikasema hivi kutoka mbinguni: "Unaambiwa hivi, Ee Mfalme Nebukadneza, 'Ufalme umekuponyoka,^a **32** nawe unafukuzwa mbali kutoka kati ya wanadamu. Utaishi na wanayama wa mwituni, nawe utapewa majani ule kama ng'ombe dume, na nyakati saba zitapita, mpaka utakapojua kwamba Aliye Juu Zaidi ni Mtawala katika ufalme wa wanadamu na yeye humpa ufalme huo yeyote anayetaka kumpa."^b

33 Papo hapo, maneno hayo yakatimia kwa Nebukadneza. Akafukuzwa mbali kutoka kati ya wanadamu, akaanza kula majani kama ng'ombe dume, na mwili wake ukalowa kwa umande wa mbinguni, mpaka nywele zake zikawa ndefu kama manyoya ya tai na kucha zake zikawa kama kucha za ndege.^c

34 "Mwishoni mwa kipindi hicho,^d mimi, Nebukadneza, nilitazama juu mbinguni, na ufahamu wangu ukanirudia; nami nikamsifu Aliye Juu Zaidi, nikamsifu na kumtukua Yeye anayeishi milele, kwa sababu utawala wake ni utawala wa milele na ufalme wake ni wa kizazi baada ya kizazi.^e **35** Wakaaji wote wa dunia wanaonwa kuwa si kitu, naye hufanya kulingana na mapeenzi yake mwenyewe miongoni mwa jeshi la mbinguni na wakaaji wa dunia. Na hakuna ye-

SURA YA 4

a Da 4:25
Mdo 12:22, 23

b Da 4:17

c Da 4:25

d Da 4:16

e Zb 10:16
Da 4:3

Safu ya 2

a Ayu 34:24
Isa 43:13

b Isa 45:9

c Da 4:26

d Da 4:2, 3

e Kum 32:4
Zb 33:5

f Kut 18:10, 11
Yak 4:6

SURA YA 5

g Da 7:1
Da 8:1

h Isa 21:5
Yer 51:39

i 2Fa 25:15
2Nya 36:18
Ezr 1:7
Yer 52:19
Da 1:1, 2

yote anayeweza kumzuia^{*a} au kumuuliza, 'Umefanya nini?'"^b

36 "Wakati huo ufahamu wangu ukanirudia, nami nika-rudiwa na utukufu wa ufalme wangu, ukuu wangu, na fahari yangu.^c Maofisa wangu wakuu na watu mashuhuri walinitafuta kwa bidii, nami nikarudishwa kwenye ufalme wangu, na hata nikaongezewa ukuu mwingi zaidi.

37 "Sasa mimi, Nebukadneza, ninamsifu na kumkweza na kumtukua Mfalme wa mbinguni,^d kwa sababu kazi zake zote ni kweli na njia zake ni haki,^e na kwa sababu ana-weza kuwaaibisha wale wa-naotembea katika kiburi."^f

5 Basi Mfalme Belshaza^g alifanya karamu kubwa kwa ajili ya wakuu wake elfu moja, naye alikuwa akinywa divai mbele yao.^h **2** Alipokuwa amelewa, Belshaza akaagiza vyombo vya dhahabu na vya fedha ambavyo Nebukadneza baba yake alikuwa amevichukua kutoka katika hekalu la Yerusalemu viletwe,ⁱ ili avitumie kunywea divai pamoja na wakuu wake, masuria wake, na wake zake wadogo.

3 Basi wakaleta vyombo vya dhahabu vilivyochukuliwa kutoka katika hekalu la Mungu kule Yerusalemu, na mfalme pamoja na wakuu wake, masuria wake na wake zake wadogo wakavitumia kunywea divai. **4** Wakanywa divai, nao wakaisifu miungu ya dhahabu na fedha, ya shaba, chuma, miti, na mawe.

5 Wakati huohuo, vidole vya mkono wa mwanadamu vikatokea na kuanza kuandika

4:35 *Au "kuuzuia mkono wake."

kwenye lipu ya ukuta wa jumba la mfalme unaoelekeana na kinara cha taa, na mfalme aliweza kuona sehemu ya nyuma ya mkono huo ulipokuwa ukiandika. **6** Ndipo uso wa mfalme ukabadilika rangi* na mawazo yake yakamwogopesha, kiuno chake kikalegea^a na magoti yake yakaanza kugongana.

7 Mfalme akawaita kwa sauti kubwa watu wanaofanya mazingaombwe, Wakaldayo,* na wanajimu.^b Mfalme akawambia wanaume hao wenye hekima wa Babiloni: "Mtu yeyote atakayesoma maandishi haya na kuniambia maana yake atavishwa mavazi ya zambarau na mkufu wa dhahabu shingoni mwake,^c naye atakuwa mtawala wa tatu katika ufalme."^d

8 Basi wanaume wote wenye hekima wa mfalme wakaja, lakini hawakuweza kusoma maandishi hayo wala kumwambia mfalme maana yake.^e **9** Kwa hiyo Mfalme Belshaza akaogopa sana na uso wake ukazidi kubadilika rangi; na wakuu wake wakapigwa na bumvuazi.^f

10 Malkia aliposikia maneno ya mfalme na wakuu wake, akaingia kwenye ukumbi wa karamu. Malkia akasema: "Ee mfalme, uishi milele. Usiruhusu mawazo yako yakuogopeshe, wala usiruhusu uso wako ubadilike rangi. **11** Kuna mwanamume fulani^g katika ufalme wako aliye na roho ya miungu mitakatifu. Katika siku za baba yako, mwana-

5:6 *Au "sura ya mfalme ikabadilika."
5:7, 11 *Yaani, wabashiri na wanajimu hodari. 5:11 ^gAu "mwanamume mwenye uwezo."

SURA YA 5

a Isa 21:2, 3

b Da 2:2
Da 4:6c Mwa 41:39, 42
Est 8:15

d Da 2:6, 48

e Da 2:27
Da 4:7

f Isa 13:1, 7

Safu ya 2

a Da 4:8, 9

b Da 2:47, 48

c Da 1:7
Da 4:8d Da 1:17, 20
Da 6:3e 2Fa 24:11, 14
Da 1:3, 6
Da 2:25

f Da 4:9

g Da 1:17, 20

h Isa 47:12, 13
Da 2:10, 11
Da 5:8

i Da 2:28

j Da 2:6
Da 5:7

mume huyo alithibitika kuwa na ujuzi na ufahamu na hekima kama hekima ya miungu.^a Baba yako Mfalme Nebukadneza alimweka kuwa mkuu wa makuhani wachawi, watu wanaofanya mazingaombwe, Wakaldayo,* na wanajimu;^b hivyo ndivyo alivyofanya baba yako, Ee mfalme. **12** Kwa maana Danieli, ambaye mfalme alimwita Belteshaza,^c alikuwa na roho isiyo ya kawaida na ujuzi na ufahamu wa kueleza maana ya ndoto, kufumbua mafumbo, na kutatua matatizo magumu.*^d Basi agiza Danieli aitwe, atakwambia maana ya maandishi haya."

13 Kwa hiyo Danieli akalemtwa mbele ya mfalme. Mfalme akamuuliza Danieli: "Je, wewe ndiye Danieli, mmojawapo wa watu waliohamishwa na baba yangu mfalme kutoka Yuda?"^e **14** Nimesikia kukuhusu kwamba roho ya miungu imo ndani yako^f na kwamba una ujuzi na ufahamu na hekima isiyo ya kawaida.^g **15** Sasa wanaume wenye hekima na watu wanaofanya mazingaombwe waliletwa mbele yangu ili wasome maandishi haya na kuniambia maana yake, lakini wameshindwa kuniambia maana ya ujumbe huu.^h **16** Lakini nimesikia kukuhusu kwamba una-weza kueleza maana ya mafumboⁱ na kutatua matatizo magumu.* Sasa, ukifaulu kusoma maandishi haya na kuniambia maana yake, utavishwa mavazi ya zambarau na mkufu wa dhahabu shingoni mwako, nawe utakuwa mtawala wa tatu katika ufalme."^j

5:12, 16 *Tnn., "kufungua mafundo."

17 Ndipo Danieli akamwambia mfalme: “Si lazima uni-pe zawadi zako, unaweza kuwapa wengine zawadi hizo. Hata hivyo, nitakusomea maandishi haya na kukuambia maana yake. 18 Ee mfalme, Mungu Aliye Juu Zaidi alimpa baba yako Nebukadneza ufalme na ukuu na heshima na fahari.^a 19 Kwa sababu ya ukuu ambao Mungu alimpa, watu wa makabila yote, mataifa, na lugha walitetemeka kwa woga mbele yake.^b Yeyote ambaye mfalme alitaka kumuua, alimuua, yeyote aliyetaka kumwacha hai, alimwacha hai, yeyote aliyetaka kumkweza, alimkweza, na yeyote aliyetaka kumwaibisha, alimwaibisha.^c 20 Lakini moyo wake ulipokuwa na kiburi na roho yake kuwa ngumu hivi kwamba akatenda kwa kimbelembele,^d alishushwa chini kutoka kwenye kiti chake cha ufalme, naye akanyang’anya heshima yake. 21 Alifukuzwa mbali kutoka kati ya wanadamu, na moyo wake ukafanywa kuwa kama wa mnyama, akaishi na punda mwitu. Alipewa majani ale kama ng’ombe dume, na mwili wake ukalowa umande wa mbinguni, mpaka alipojua kwamba Mungu Aliye Juu Zaidi ni Mtawala katika ufalme wa wanadamu na kwamba yeye humweka yeyote amtakaye juu ya ufalme huo.^e

22 “Lakini wewe Belshaza, mwanawe, hujaunyenyekeza moyo wako, ingawa ulijua hayo yote. 23 Badala yake, uljikweza mwenyewe dhidi ya Bwana wa mbinguni,^f ukawaamuru wakulettee vyombo vya nyumba yake.^g Kisha wewe pa-

SURA YA 5

a Da 2:37, 38

b Yer 25:9
Da 3:4, 5
Da 4:22c Da 2:12
Da 3:6, 29d Isa 14:13, 14
Da 4:30

e Da 4:31-35

f Yer 50:29

g Da 5:2, 3

Safu ya 2

a Zb 115:4-7
Isa 46:6, 7

b Zb 104:29

c Da 5:5

d Isa 13:11
Yer 25:12
Yer 27:6, 7
Yer 50:1, 2
Yer 51:11e Ezz 1:1, 2
Isa 21:2
Isa 45:1
Yer 50:9
Da 6:28
Da 9:1

f Da 5:7, 16

g Isa 21:9
Yer 51:8, 31
Yer 51:39, 57h Da 6:1
Da 9:1

SURA YA 6

i Est 1:1
Da 9:1j Da 2:48
Da 5:29k Ezz 8:36
Est 8:9
Da 3:2

moja na wakuu wako, masuria wako, na wake zako wadogo mkavitumia kunywea di-vai na kuisifu miungu ya fedha na ya dhahabu, ya shaba, chuma, miti, na mawe, miungu ambayo haioni chochote na haisikii chochote na haijui chochote.^a Lakini hujamtukuzza Mungu ambaye pumzi yako na njia zako zote zimo mikononi mwake.^b 24 Kwa hiyo yeye ndiye aliyeutuma mkonu huo, na maandishi haya yakaandikwa ukutani.^c 25 Na haya ndiyo maandishi yaliyoandikwa: MENE, MENE, TEKE-LI, na PARSINI.

26 “Hii ndiyo maana ya maneno hayo: MENE, Mungu amehesabu siku za ufalme wako na kuukomesha.^d

27 “TEKELI, umepimwa katika mizani na kuonekana umepungukiwa.

28 “PERESI, ufalme wako umegawanywa wakapewa Wamedi na Waajemi.”^e

29 Ndipo Belshaza akatoa amri, nao wakamvisha Danieli mavazi ya zambarau na mku-fu wa dhahabu shingoni mwake; wakatangaza kwamba atakuwa mtawala wa tatu katika ufalme.^f

30 Usiku huohuo Belshaza mfalme wa Wakaldayo aliuawa.^g 31 Na Dario^h Mmedi akaupokea ufalme; alikuwa na umri wa miaka 62 hivi.

6 Mfalme Dario aliona vema kuwaweka maliwali 120 kusimamia ufalme wake wote.ⁱ

2 Juu yao kulikuwa na maofisa watatu wakuu, Danieli/ alikuwa mmoja wao; na maliwali^k walikuwa wakiwapelekea habari, ili mfalme asipate hasara. 3 Sasa, Danie-

li alijidhihirisha kuwa tofauti na wale maofisa wengine wakuu na maliwali, kwa maana roho isiyo ya kawaida ilikuwa ndani yake,^a na mfalme alikusudia kumkweza juu ya ufalme wote.

4 Wakati huo maofisa wakuu na maliwali walikuwa wakitafuta msingi fulani wa kumshtaki Danieli kuhusiana na mambo ya serikali,* lakini hawakuweza kupata msingi wowote wa kumshtaki wala ufisadi wowote, kwa sababu alikuwa mwenye kutegemeka, naye hakupatikana kamwe akiwa mzembe wala mfasidi. **5** Ndipo wanaume hao wakasema: “Hatutapata msingi wowote wa kumshtaki huyu Danieli, isipokuwa tutafute msingi wa kumshtaki kuhusiana na sheria ya Mungu wake.”^b

6 Basi maofisa hao wakuu na maliwali wakaenda wakiwa kikundi kwa mfalme na kumwambia: “Ee Mfalme Dario, uishi milele. **7** Maofisa wote wa mfalme, wasimamizi, maliwali, maofisa wakuu wa mfalme, na magavana, wameshauriana ili mfalme atoe amri na kutangaza marufuku, kwamba kwa siku 30 mtu yeye atakayemwomba mungu yeyote au mwanadamu isipokuwa wewe, Ee mfalme, anapaswa kutupwa ndani ya shimo la simba.”^c **8** Na sasa, Ee mfalme, itoe amri hiyo na kuitia sahihi,^d ili isiweze kubadilisha kulingana na sheria ya Wamedi na Waajemi, ambayo haiwezi kufutwa.”^e

9 Kwa hiyo Mfalme Dario akatia sahihi amri hiyo na marufuku hayo.

SURA YA 6

a Da 1:17, 20
Da 5:12

b Est 3:8

c Da 3:6

d Est 3:12
Est 8:10e Est 1:19
Est 8:8

Safu ya 2

a 1Fa 8:44, 45

b Est 8:8
Da 6:7, 8c Da 1:3, 6
Da 2:25
Da 5:13d Est 3:8
Da 6:10

10 Lakini mara tu Danieli alipojua kwamba amri hiyo imetiwa sahihi alienda nyumbani kwake, na madirisha ya chumba chake kilichokuwa darini yalikuwa yamefunguliwa kuelekea Yerusalem.^a Na mara tatu kwa siku alipiga magoti na kusali na kumsifu Mungu wake, kama alivyokuwa akifanya kwa ukawaida kabla ya mambo hayo. **11** Wakati huo wanaume hao wakaingia kwa kishindo na kumkuta Danieli akimwomba na kumsihi Mungu wake apate kibali mbele zake.

12 Kwa hiyo wakaenda kwa mfalme na kumkumbusha kuhusu marufuku aliyotangaza: “Je, hukutia sahihi marufuku ukisema kwamba kwa siku 30 mtu yeyote atakayemwomba mungu yeyote au mwanadamu yeyote isipokuwa wewe, Ee mfalme, anapaswa kutupwa ndani ya shimo la simba?” Mfalme akasema: “Hivyo ndivyo ilivyo kulingana na sheria ya Wamedi na Waajemi, isiyoweza kufutwa.”^b **13** Mara moja wakamwambia mfalme: “Danieli, mmoja wa watu waliohamishwa kutoka Yuda^c hakuheshimu wewe, Ee mfalme, wala marufuku uliyotia sahihi, badala yake anasali mara tatu kwa siku.”^d **14** Mara tu mfalme aliposikia hivyo, alihuzunika sana, akajaribu kutafuta njia ya kumwokoza Danieli; alifanya kila jitihada ya kumwokoza mpaka jua likatua. **15** Mwishowe wanaume hao wakaenda mbele ya mfalme wakiwa kikundi na kumwambia: “Ee mfalme, zingatia kwamba sheria ya Wamedi na Waajemi inasema kwamba marufuku yoyote au amri yoyote

6:4 * Tnn., “ufalme.”

iliyowekwa na mfalme haiwezi kubadilishwa.”^a

16 Basi mfalme akatoa agizo, nao wakamleta Danieli na kumtupa ndani ya shimo la simba.^b Mfalme akamwambia Danieli: “Mungu wako unayemtumikia daima, atakuokoa.”

17 Kisha jiwe likaletwa na kuwekwa kwenye mwingilio* wa shimo hilo, naye mfalme akalitia muhuri kwa pete yake ya muhuri na kwa pete ya muhuri ya wakuu wake ili uamuzi kumhusu Danieli usibadilishwe hata kidogo.

18 Kisha mfalme akaenda kwenye jumba lake la kifalme. Akafunga usiku kucha na kukataa kutumbuizwa kwa njia yoyote,* naye akashindwa kulala usingizi.[#] **19** Hatimaye, alfajiri na mapema, mfalme aliondoka na kwenda haraka kwenye lile shimo la simba. **20** Alipokaribia shimo hilo, akamwita Danieli kwa sauti ya huzuni. Mfalme akamuuliza Danieli: “Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je, Mungu wako unayemtumikia daima ameweza kukuokoa kutoa kwa simba hao?” **21** Mara moja Danieli akamjibu mfalme: “Ee mfalme, uishi milele. **22** Mungu wangu alimtumalaika wake akafunga vinywa vya simba,^c nao hawanidhuru,^d kwa sababu siku-patikana na hatia mbele zake; wala sijakutendea jambo lolote baya, Ee mfalme.”

23 Mfalme akafurahi sana, akaamuru Danieli atolewe ndani ya lile shimo. Danieli alipotolewa shimoni, hakuwa

6:17 *Tnn., “mdomo.” 6:18 *Au labda, “hakuna wanamuziki walioletwa.”^a Tnn., “usingizi ulimkimbia.”

SURA YA 6

a Est 8:8
Da 6:8

b Da 6:7
Ebr 11:32, 33

c 1Sa 17:37
Ebr 11:32, 33

d Zb 34:7
Zb 118:5
Da 3:28

Safu ya 2

a Zb 37:40
Met 18:10
Da 3:26, 27

b Est 7:10

c Est 8:9
Da 4:1

d Da 3:29

e Da 4:34

f Da 3:28

g Yer 32:20
Da 4:3

h Da 5:31
Da 6:1, 2

i 2Nya 36:22, 23
Ezr 1:1, 2
Isa 44:28

SURA YA 7

j Da 5:1, 30

k Da 2:19
Da 8:1

l Isa 30:8
Hab 2:2
Ufu 1:11

amepatwa na madhara yoyote, kwa sababu alikuwa amemtumaini Mungu wake.^a

24 Kisha mfalme akatoa agizo, na wanaume waliokuwa wamemshtaki* Danieli wakaletwa, nao wakatupwa ndani ya lile shimo la simba, pamoja na wake zao na watoto wao. Kabla hawajafika chini shimoni, simba waliwashinda nguvu na kuvunjavunja mifupa yao yote.^b

25 Kisha Mfalme Dario akaandikia watu wa makabila yote, mataifa, na lugha wanaokaa katika dunia yote:^c “Muwe na amani tele! **26** Ninatoa agizo kwamba katika kila eneo la ufalme wangu, watu wanapaswa kutetemeka kwa woga mbele za Mungu wa Danieli.^d Kwa maana yeye ndiye Mungu aliye hai naye huishi milele. Ufalme wake hautangamizwa kamwe, na utawala wake ni wa* milele.^e **27** Yeye huokoa,^f naye hufanya ishara na maajabu mbinguni na duniani,^g kwa sababu alimwokoa Danieli kutoka katika makucha ya simba.”

28 Basi Danieli huyo akafanikiwa katika ufalme wa Dario^h na katika ufalme wa Koreshi Mwajemi.ⁱ

7 Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Mfalme Belshaza/ wa Babiloni, Danieli aliota ndoto na kuona maono akiwa amelala kitandani mwake.^k Kisha akaandika ndoto hiyo,^l akaandika masimulizi kamili ya mambo hayo. **2** Danieli akasema:

“Nilikuwa nikitazama katika maono yangu wakati wa usi-

6:24 *Au “waliomchongea.” 6:26 *Au “enzi yake ni ya.”

ku, na tazama! pepo nne za mbingu, zilikuwa zikivuruga bahari kubwa sana.^a **3** Na wanyama wanne^b wakubwa sana wakatoka katika bahari hiyo, kila mmoja alikuwa tofauti na wenzake.

4 “Wa kwanza alikuwa kama simba,^c naye alikuwa na mabawa ya tai.^d Nikatazama mpaka mabawa yake yakang’olewa, akainuliwa kutoka duniani na kusimamishwa kwa miguu miwili kama mwanadamu, naye akapewa moyo wa mwanadamu.

5 “Na tazama! mnyama mwingine, wa pili, kama dubu.^e Aliinuliwa upande mmoja, na mbavu tatu zilikuwa kinywani mwake kati ya meno yake; naye akaambiwa, ‘Sima, kula nyama nyingi.’^f

6 “Baada ya hayo nikaendelea kuangalia, na tazama! mnyama mwingine, kama chui,^g lakini mgongoni mwake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege. Na mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne,^h naye alipewa mamlaka ya kutawala.

7 “Baada ya hayo nikaendelea kutazama katika maono ya usiku, nikaona mnyama wa nne, mwenye kuogopesha na mwenye kutisha, na mwenye nguvu isivyo kawaida, naye alikuwa na meno makubwa ya chuma. Alikuwa akinyafua na kuvunjavunja, na kili-chobaki alikikanyaga-kanyaga chini kwa miguu yake.ⁱ Alikuwa tofauti na wanyama wote waliomtangulia, naye alikuwa na pembe kumi. **8** Nilipokuwa nikiangalia pembe hizo, tazama! pembe wengine, ndogo,^j ikajitokeza miongoni mwa

SURA YA 7

- a Isa 57:20
Ufu 17:15
b Da 7:17
c Da 2:37, 38
d Kum 28:49, 50
Yer 48:40
Omb 4:19
Hab 1:8
e Da 2:39
Da 5:28
Da 8:3, 20
f Isa 13:17, 18
Da 11:2
g Da 2:39
Da 8:5
Da 11:3
h Da 8:8
Da 11:4
i Da 2:40
Da 7:19
j Da 7:24

Safu ya 2

- a Da 7:20
Ufu 13:5
b Zb 90:2
Da 7:13, 22
Hab 1:12
c Isa 6:1, 2
Ufu 4:2, 3
d Zb 104:1, 2
e Kum 9:3
Ebr 12:29
f Zb 50:3
Zb 97:3
g Kum 33:2
1Fa 22:19
Zb 68:17
Ebr 12:22
Yud 14
Ufu 5:11
h 1Sa 2:10
Zb 50:6
i Da 7:8, 25
j Da 7:3
k Mt 24:30
Lu 21:27
Yoh 3:13
Mdo 7:56
Ufu 14:14
l Zb 90:2
Da 7:9, 22
Hab 1:12
m Zb 2:6
Zb 110:1, 2
Mt 28:18
1Ko 15:25
Efe 1:22
Ufu 3:21
n Flp 2:9-11
o Mwa 49:10

pembe hizo, na pembe tatu kati ya zile za kwanza zikang’olewa mbele yake. Na, tazama! pembe hiyo ilikuwa na macho kama ya mwanadamu, na ilikuwa na kinywa kinachozungumza kwa kiburi.^{*a}

9 “Nikaendelea kutazama mpaka viti vya ufalme vikawekwa na Mzee wa Siku^b akaketi.^c Mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji,^d na nywele za kifwacha chake zilikuwa kama safu safi. Kiti chake cha ufalme kilikuwa miali ya moto; magurudumu yake yalikuwa moto unaowaka.^e **10** Mto wa moto ulikuwa ukitiririka kutoka mbele zake.^f Elfu kwa maelfu waliendelea kumhudumia, na elfu kumi mara elfu kumi walisimama mbele zake.^g Mahakama^h ikaketi, na vitabu vikafunguliwa.

11 “Nikaendelea kutazama wakati huo kwa sababu ya mvumo wa maneno ya kiburi* yaliyokuwa yakisemwa na pembe hiyo;ⁱ nilitazama mpaka mnyama huyo alipouawa na mwili wake ukaharibiwa na kutolewa ili uchomwe moto. **12** Lakini wale wanyama wengine^j walinyang’anywa tawala zao, na maisha yao yakarefushwa kwa wakati mmoja na majira.

13 “Nikaendelea kuangalia katika maono ya usiku, na tazama! mtu fulani kama mwana wa binadamu^k alikuwa aki-ja na mawingu ya mbinguni; naye akaja mbele za Mzee wa Siku,^l nao wakamleta karibu Naye. **14** Naye akapewa utawala,^m heshima,ⁿ na ufalme, ili watu wa makabila, mataifa, na lugha zote wantumikie.^o

7:8, 11 *Au “kujigamba.”

Utawala wake ni utawala wa milele ambao hautapitilia mbali, na ufalme wake hautaangamizwa.^a

15 “Basi, mimi Danieli, roho yangu ilifadhaika kwa sababu maono ya kichwa changu yalinigopesha.^b **16** Nikamkaribia mmoja wa wale waliokuwa wamesimama pale ili nimuulize maana halisi ya mambo hayo. Basi akanijibu na kunieleza maana ya mambo hayo.

17 “Wanyama hawa wakubwa, wanne,^c ni wafalme wanne ambao watasimama kutoka duniani.^d **18** Lakini watakatifu wa Aliye Mkuu Zaidi^e watapokea ule ufalme,^f nao wataumiliki ufalme huo^g milele, naam, milele na milele.’

19 “Kisha nikataka kujua mengi zaidi kuhusu yule mnyama wa nne, ambaye alikuwa tofauti na wale wengine; alikuwa mwenye kuogopesha isivyo kawaida; alikuwa na meno ya chuma na makucha ya shaba, naye alikuwa akinyafua na kuvunjavunja, na kukanyaga-kanyaga chini kwa miguu yake kilichobaki;^h **20** na pia kuhusu zile pembe kumiⁱ zilizokuwa kichwani mwake, na ile pembe nyingine iliyojitokeza na ambayo mbele yake pembe tatu zilianguka,^j pembe iliyokuwa na macho na kinywa kilichozungumza kwa kiburi* na ambayo umbo lake lilikuwa kubwa kuliko umbo la zile pembe nyingine.

21 “Nikaendelea kutazama pembe hiyo ilipokuwa ikiwapiga vita watakatifu, nayo ilikuwa ikiwashinda,^k **22** mpaaka Mzee wa Siku^l alipokuja na

7:20 *Au “kwa kujigamba.”

SURA YA 7

a Zb 45:6
Isa 9:6, 7
Da 2:44
Lu 1:32, 33
Ufu 11:15

b Da 8:27

c Da 7:3

d Da 2:39, 40

e Da 7:25, 27

f Mt 19:28
ZTi 2:12
Ufu 3:21
Ufu 5:9, 10

g Da 7:21, 22
Lu 22:29

h Da 2:40
Da 7:7

i Da 7:24

j Da 7:8

k Da 8:23, 24
Da 12:7
Ufu 13:7

l Zb 90:2
Da 7:9, 13
Hab 1:12

Safu ya 2

a Da 7:18, 27

b Mt 19:28
Lu 22:29
Ufu 1:6
Ufu 3:21
Ufu 5:9, 10
Ufu 20:4

c Da 2:40
Da 7:7

d Da 7:20

e Da 7:8

f Da 12:7
Ufu 13:5-7

g Da 7:10, 11

h Da 7:22
Mt 19:28
Lu 22:29
Ufu 20:4

i Ufu 11:15

kuhukumu kwa faida ya watakatifu wa Aliye Mkuu Zaidi,^a na wakati uliowekwa ukafika wa watakatifu kuumiliki ufalme.^b

23 “Alisema hivi: ‘Kuhusu yule mnyama wa nne, kuna ufalme wa nne utakao tokea duniani. Utakuwa tofauti na falme nyingine zote, nao utainyafua dunia yote na kuikanyaga-kanyaga chini na kuivunjavunja.^c **24** Kuhusu zile pembe kumi, wafalme kumi watainuka kutoka katika ufalme huo; na bado kuna mwingine atakayeinuka baada yao, atakuwa tofauti na wale wa kwanza, naye atawaabisha wafalme watatu.^d

25 Atasema maneno dhidi ya Aliye Juu Zaidi,^e naye ataeendelea kuwanyanyasa watakatifu wa Aliye Mkuu Zaidi. Atakusudia kubadili nyakati na sheria, nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, nyakati, na nusu wakati.^{*f} **26** Lakini ile Mahakama ikaketi, nao wakamnyang’anya utawala wake, ili wamwagamize na kumharibu kabisa.^g

27 “Na ufalme na utawala na utukufu wa falme chini ya mbingu zote ulikabidhiwa watu ambao ni watakatifu wa Aliye Mkuu Zaidi.^h Ufalme wao ni ufalme wa milele,ⁱ na tawala zote zitawatumikia na kuwatii wao.’

28 “Huu ndio mwisho wa jambo hilo. Basi mimi, Danieli, mawazo yangu yalinigopesha sana, hivi kwamba uso wangu ukabadilika* rangi; lakini niliweka jambo hilo katika moyo wangu mwenyewe.”

7:25 *Yaani, nyakati tatu na nusu.

7:28 *Au “sura yangu ikabadilika.”

8 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Mfalme Belshaza,^a mimi, Danieli, niliona maono, baada ya yale niliyoona mwanzoni.^b **2** Niliona maono hayo, na nilipokuwa nikiyaona nilikuwa katika ngome ya* Shushani,^c iliyo katika mkoa wa^d Elamu;^d niliona maono hayo, nami nilikuwa kando ya mfereji wa maji wa Ulai. **3** Nilipoinua macho yangu, tazama! kulikuwa na kondoo dume^e aliyesimama mbele ya mfereji huo wa maji, naye alikuwa na pembe mbili.^f Pembe hizo mbili zilikuwa ndefu, lakini moja ilikuwa ndefu kuliko nyingine, na pembe hiyo ndefu ilitokea baadaye.^g **4** Nikamwona huyo kondoo dume akisonga mbele kwa nguvu kuelekea magharibi, kaskazini, na kusini, na hakuna mnyama yeyote wa mwituni aliyeweza kusimama mbele yake, wala hakukuwa na yeyote aliyeweza kuokoa kutoka katika nguvu zake.^h Alifanya apendavyo na kujikweza.

5 Nilipokuwa nikiendelea kuangalia, tazama! kulikuwa na mbuzi dumeⁱ aliyekuwa akija kutoka magharibi* akivuka dunia yote bila kugusa ardhi. Na mbuzi huyo alikuwa na pembe iliyoonekana waziwazi kati ya macho yake.^j **6** Alikuwa akija kumwelekea yule kondoo dume mwenye pembe mbili ambaye nilimwona amesimama mbele ya ule mfereji wa maji; alikuwa akikimbia kumwelekea kwa ghadhabu kubwa.

8:2 *Au "jumba la mfalme la." ^aAu "Susa." ^bAu "wilaya ya utawala ya." 8:4, 7 *Tnn., "mkono wake." 8:5 *Au "machweo ya jua."

SURA YA 8

a Da 5:1, 30

b Da 7:1, 15

c Ne 1:1
Est 2:8d Mwa 10:22
Isa 11:11
Isa 21:2e Isa 13:17
Yer 51:11
Da 7:5
Da 8:20

f Est 1:1, 3

g Isa 44:28

h Isa 45:1
Yer 51:12
Da 5:30, 31i Da 2:39
Da 7:6
Da 8:21

j Da 11:3

Safu ya 2

a Da 8:22
Da 11:4b Zb 48:2
Da 11:16, 45c Da 11:31
Da 12:11

7 Nikamwona akimkaribia yule kondoo dume, naye alikuwa amejawa na uchungu mwingi kumwelekea. Akampiga na kumwangusha chini huyo kondoo dume na kuzivunja pembe zake mbili, na kondoo dume huyo hakuwa na nguvu za kustahimili. Basi akamwangusha ardhini kondoo dume huyo na kumkanyaganyaga, na hakukuwa na yeyote wa kumwokoia kutoka katika nguvu zake.*

8 Kisha huyo mbuzi dume akajikweza kupita kiasi, lakini mara tu alipokuwa na nguvu, ile pembe kubwa ikavunjika; kisha mahali pake zikatokea pembe nne zilizokuwa zikionekana waziwazi, kuelekea zile pepo nne za mbingu.^a

9 Pembe nyingine ndogo ilitokea katika mojawapo ya pembe hizo, nayo ikakua ikawa kubwa sana kuelekea kusini na kuelekea mashariki* na kuelekea lile Pambo.^b **10** Ikawa kubwa sana hivi kwamba ikalifikia jeshi la mbinguni, nayo ikasababisha sehemu ya jeshi hilo na baadhi ya nyota zianguke duniani, nayo ikazikanyaga-kanyaga.

11 Ikajikweza hata dhidi ya Mkuu wa jeshi hilo, na ile dhabihu inayotolewa daima ikaoondolewa* kutoka kwake, na mahali pake patakatifu palipo imara pakatupwa chini.^c **12** Na kwa sababu ya uasi, jeshi likatiwa mikononi mwa pembe hiyo, pamoja na ile dhabihu inayotolewa daima,* nayo iliendelea kuutupa ukweli duniani, ikatenda na kufanikiwa.

8:9 *Au "mawio ya jua." ^aAu "ule Urembo." 8:11 *Au "kile kitu kinachotolewa kila siku kikaondolewa." 8:12 *Au "kile kitu kinachotolewa kila siku."

13 Nami nikamsikia mta-
katifu akizungumza, na mta-
katifu mwingine akamuuli-
za mtakatifu aliyekuwa aki-
zungumza: "Maono ya dhabi-
hu inayotolewa daima* na
ya uasi unaosababisha ukiwa
yataendelea kwa muda gani^a
kufanya mahali patakati-
fu na lile jeshi kuwa vitu
vya kukanyagwa-kanyagwa?"

14 Basi akaniambia: "Kwa
muda wa jioni na asubuhi
2,300; na hakika mahali pa-
takatifu patarudishwa katika
hali yake inayofaa."

15 Mimi, Danieli, nilipoku-
wa nikiona maono hayo na ku-
jaribu kuyaelewa, kwa gha-
fla nikamwona mtu fulani ali-
yeonekana kama mwanamu-
me amesimama mbele yangu.

16 Kisha nikasikia sauti ya
mwanamume katikati ya mfe-
reji wa Ulai,^b akaita kwa sau-
ti kubwa: "Gabrieli,^c mwele-
weshe mtu huyo mambo ali-
yoona."^d **17** Kwa hiyo aka-
karibia mahali nilipokuwa
nimesimama, lakini alipoku-
ja niliogopa sana hivi kwa-
mba nikaanguka chini kifud-
difi. Akaniambia: "Elewa,
Ee mwana wa binadamu, kwa-
mba maono hayo ni ya wakati
wa mwisho."^e **18** Lakini ali-
pokuwa akizungumza nami,
nilishikwa na usingizi mzito
huku nikiwa nimeanguka chi-
ni kifudifi. Basi akanigu-
sa na kunisimamisha mahali
nilipokuwa nimesimama mwa-
nzoni.^f **19** Kisha akasema:
"Ninakujulisha yatakayotokea
katika sehemu ya mwisho ya
shutuma, kwa sababu maono
hayo yanahusu wakati uliowe-
kwa wa mwisho."^g

8:13 *Au "kile kitu kinachotolewa kila
siku."

SURA YA 8

a Da 12:11

b Da 8:2

c Lu 1:19, 26

d Da 9:21, 22

e Da 10:14
Da 12:4, 9

f Da 10:9, 10

g Da 11:27

Safu ya 2

a Da 7:5
Da 8:3
Da 11:2

b Da 7:6

c Da 8:5
Da 11:3d Da 8:8
Da 11:4e Da 7:25
Da 8:10

f Da 10:14

20 "Yule kondoo dume
mwenye pembe mbili uli-
yemwona anafananisha wa-
falme wa Umedi na Uajemi.^a

21 Yule mbuzi dume mwenye
manyoya anafananisha mfal-
me wa Ugiriki;^b na ile pembe
kubwa iliyokuwa kati ya ma-
cho yake, inafananisha mfal-
me wa kwanza.^c **22** Kuhusu
ile pembe iliyovunjika, kisha
pembe nne zikatokea badala
yake,^d kuna falme nne kuto-
ka katika taifa lake zitakazo-
simama, lakini hazitakuwa na
nguvu kama zake.

23 "Na katika kipindi cha
mwisho cha ufalme wao, waa-
si watakapofikia kilele cha ku-
tenda maovu, mfalme mwe-
nye uso mkali anayeelewa
mafumbo* atatokea. **24** Ata-
kuwa na nguvu nyingi, laki-
ni si kwa uwezo wake mwe-
nyewe. Ataleta uharibifu kwa
njia isiyu ya kawaida,* naye
atafanikiwa katika kila analo-
tenda. Atawaangamiza wenye
nguvu, na pia watu watakati-
fu.^e **25** Na kwa ujanja wake
atatumia udanganyifu kufa-
nikiwa; na katika moyo wake
atajikweza; na atawaangami-
za watu wengi wakati wa usa-
lama.* Hata atasimama dhi-
di ya Mkuu wa wakuu, lakini
atavunjwa si kwa mkono wa
mwanadamu.

26 "Mambo yaliyosemwa
katika maono kuhusu jioni na
asubuhi hizo ni ya kweli, laki-
ni ni lazima uyaweke siri ma-
ono hayo, kwa sababu yanahu-
su kipindi cha siku nyingi ku-
toka sasa."^{**f}

8:23 *Au "aliye stadi wa hila." **8:24**
*Au "Ataleta uharibifu wa kutisha."
8:25 *Au labda, "bila onyo." **8:26** *Au
"wakati ujao ulio mbali."

27 Basi mimi, Danieli, nilichoka sana nikawa mgonjwa kwa siku kadhaa.^a Kisha nikaamka na kufanya kazi ya mfalme;^b lakini mambo niliyokuwa nimeona yalifanya nife ganzi, na hakuna yeyote aliyeweza kuelewa maono hayo.^c

9 Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Dario^d mwana wa Ahasuero—mzao wa Wamedi aliyekuwa amewekwa kuwa mfalme wa ufalme wa Wakaldayo^e— 2 katika mwaka wa kwanza wa utawala wake, mimi, Danieli, nilitambua kutokana na vitabu* idadi ya miaka iliyokuwa imetajwa katika neno la Yehova kwa nabii Yermia ili kutimiza ukiwa wa Yerusalemu,^f yaani, miaka 70.^g 3 Basi nikaigeza uso wangu kumwelekea Yehova Mungu wa kweli, nikimsihi katika sala, pamoja na kufunga^h na kuvaa nguo za magunia na kujimwagia majivu. 4 Nilisali kwa Yehova Mungu wangu, nikaungama na kusema:

“Ee Yehova Mungu wa kweli, Mungu mkuu na Mwenye kuogopesha, unayeshika agano lako na kuwatendea kwa upendo mshikamanifuⁱ wale wanaokupenda na kushika amri zako,^j 5 tumetenda dhambi na tumekosea na tumetenda uovu na kuasi;^k nasi tumegeuka na kuacha amri zako na sheria* zako. 6 Hatujawasiliza watumishi wako manabii,^l ambao kwa jina lako walizungumza na wafalme wetu, wakuu wetu, mababu zetu, na watu wote nchini. 7 Ee Yehova, uadilifu ni wako, laki-

9:2 *Yaani, vitabu vitakatifu. 9:5 *Au “hukumu.”

SURA YA 8

a Da 7:28

Da 10:16

b Da 2:48, 49

c Da 8:17

SURA YA 9

d Da 6:28

Da 11:1

e Da 5:30, 31

f Ezz 1:1, 2

Zb 79:1

Isa 64:10

Omb 1:1

g 2Nya 36:20, 21

Yer 25:11

Yer 29:10

Zek 1:12

Zek 7:5

h Ezz 8:21

i Kut 34:6

j Kum 5:9, 10

Ne 1:5

k Ezz 9:6, 7

Ne 9:26, 33

Zb 106:6

Omb 3:42

l 2Nya 36:15, 16

Yer 7:13

Safu ya 2

a Law 26:33

Kum 28:41

2Fa 17:6

Isa 11:11

b Kut 34:6, 7

Ne 9:17

Zb 86:5

c Ne 9:26

d 2Fa 17:13, 14

e Kum 28:15

Kum 31:17

f Omb 2:17

g Yer 39:8

h Law 26:16, 17

Kum 28:15

Omb 1:1

i Isa 9:13

Yer 5:3

ni aibu ni yetu kama ilivyo leo, sisi watu wa Yuda, wakaa-ji wa Yerusalemu, na Waisraeli wote, wale walio karibu na walio mbali, katika nchi zote ambazo uliwatawanya kwa sababu hawakutenda kwa uaminifu kukuelekea.^a

8 “Ee Yehova, aibu ni yetu, wafalme wetu, wakuu wetu, na mababu zetu, kwa sababu tumekutendea dhambi. 9 Rehema na msamaha ni zako Yehova Mungu wetu,^b kwa maana tumekuasi.^c 10 Hatujaitii sauti yako Yehova Mungu wetu kwa kufuata sheria zako ulizotupatia kupitia watumishi wako manabii.^d 11 Waisraeli wote wamekiuka Sheria yako na kukuacha kwa kutotii sauti yako, hivi kwamba ukatumwagia laana na kiapo kilichoandikwa katika Sheria ya Musa mtumishi wa Mungu wa kweli,^e kwa maana tumekutendea Wewe dhambi. 12 Umetimiza maneno uliyosema dhidi yetu^f na dhidi ya watawala wetu waliotutawala, * kwa kutuletea msiba mkubwa; hakuna jambo lililowahi kufanywa chini ya mbingu zote kama jambo lililofanywa Yerusalemu.^g 13 Kama tu ilivyoandikwa katika Sheria ya Musa, msiba huu wote umetujia,^h lakini hatujakuomba kibali* Yehova Mungu wetu kwa kuacha uovu wetuⁱ na kwa kuonyesha ufahamu katika ukweli^j wako.

14 “Basi Yehova ukakaa macho na kutuletea msiba, kwa maana wewe Yehova Mungu wetu ni mwadilifu katika

9:12 *Tnn., “waamuzi wetu waliotuhukumu.” 9:13 *Au “hatujautuliza uso wa.” #Au “uaminifu.”

kazi zote ambazo umefanya; hata hivyo sisi hatujaitii sauti yako.^a

15 "Sasa, Ee Yehova Mungu wetu, Wewe uliyewatoa watu wako nchini Misri kwa mkono wenye nguvu,^b na kujijengea jina hadi leo hii,^c tumefanya dhambi na kutenda uovu.

16 Ee Yehova, kulingana na matendo yako yote ya uadilifu,^d tafadhali, iondoe hasira na ghadhabu yako kutoa katika jiji lako Yerusalemu, mlima wako mtakatifu; kwa maana dhambi zetu na makosa ya mababu zetu yamefanya Yerusalemu na watu wako wawe kitu cha kushutumiwa na watu wote wanaotuzunguka.^e **17** Na sasa sikiliza, Ee Mungu wetu, sala yangu mimi mtumishi wako na maombi yangu, na ufanye uso wako uangaze juu ya mahali pako patakatifu^f palipo ukiwa,^g kwa ajili yako mwenyewe, Ee Yehova. **18** Tega sikio lako, Ee Mungu wangu, usikie! Fungua macho yako uone hali yetu ya ukiwa na jiji ambalo limeitwa kwa jina lako; kwa maana hatukuombi kwa sababu ya matendo yetu ya uadilifu bali kwa sababu ya rehemu yako kuu.^h **19** Ee Yehova, sikia. Ee Yehova, samehe.ⁱ Ee Yehova, sikiliza kwa makini na uchukue hatua. Usikawie, kwa ajili yako mwenyewe, Ee Mungu wangu, kwa maana jiji lako na watu wako wameitwa kwa jina lako mwenyewe."^j

20 Nilipokuwa bado nikiongea na kusali na kuungama dhambi yangu na dhambi ya watu wangu Waisraeli na kuomba kibali mbele za Yehova Mungu wangu kuhusu mlima

SURA YA 9

a Ne 9:33

b Kut 6:1

c Kut 9:16
Ne 9:10
Zb 106:7, 8d Zb 89:14
Isa 26:9e Law 26:38, 39
Ifa 9:7-9
Zb 79:1, 4
Yer 24:9

f Hes 6:23, 25

g Isa 64:10, 11
Omb 5:18h Zb 102:13
Isa 54:7, 8
Yer 14:7

i Ifa 8:30

j Zb 79:8, 9
Isa 63:18, 19
Yer 14:9

Safu ya 2

a Zb 87:1, 2
Zek 8:3b Da 8:16
Lu 1:19

c Da 8:1

d Da 10:11, 19

e Ne 11:1
Isa 52:1f Lu 1:76, 77
Ebr 9:26g Ro 3:25
1Yo 2:1, 2
1Yo 4:10h Isa 53:11
Ro 1:16, 17

i 2Ko 1:19, 20

j Ne 2:5, 11
Ne 6:15k Zb 2:2
Yoh 1:41l Isa 55:4
Mt 23:10
Yoh 1:45, 49

m Lu 3:1, 2

n Isa 53:8, 12
Mt 26:2
Lu 24:26
1Ko 15:3

o Mk 9:12

mtakatifu wa Mungu wangu,^a **21** naam, nilipokuwa bado nikisali, mwanamume Gabrieli,^b niliyekuwa nimemwona awali katika maono,^c alinjia nilipokuwa nimechoka kwelikweli karibu wakati ambao zawadi ya jioni hutolewa. **22** Naye akanipa uelewaji akisema:

"Ee Danieli, sasa nimekuja kukupa ufahamu na uelewaji. **23** Ulipoanza kusali jibu lilitolewa, nami nimekuja kukujulisha jibu hilo, kwa sababu wewe ni mtu mwenye thamani sana."^d Basi zingatia ujumbe huu na kuelewa maono haya.

24 "Kuna majuma 70* ambayo yameamuliwa kwa ajili ya watu wako na kwa ajili ya jiji lako takatifu,^e ili kukomesha uasi, kumaliza kabisa dhambi,^f kufunika makosa,^g kuleta uadilifu wa milele,^h kutia muhuri maono na unabii,ⁱ na kutia mafuta Patakatifu pa Patakatifu.^Δ **25** Unapaswa kujua na kuelewa kwamba tangu kutolewa kwa lile neno la kurudisha na kujenga upya Yerusalemu/ mpaka atakapotokea Masihi*^k aliye Kiongozi,^l kuta-kuwa na majuma 7, na pia majuma 62.^m Yerusalemu litarudishwa na kujengwa upya, pamoja na uwanja wa jiji na handaki, lakini katika nyakati za taabu.

26 "Na baada ya hayo majuma 62, Masihi atauawa,ⁿ hatabaki na chochote.^o

"Na watu wa kiongozi anayekuwa wataliharibu jiji na ma-

9:23 *Au "anayependwa sana; anayeheshimiwa sana." **9:24** *Yaani, majuma 70 ya miaka. #Tnn., "nabii." ΔAu "Patakatifu Zaidi." **9:25** *Au "Mtiwa-Mafuta." **9:26** *Tnn., "atakatiliwa mbali."

hali patakatifu.^a Na mwisho wake utakuwa kwa mafuriko. Na mpaka ule mwisho kutakuwa na vita; kilichoamuliwa ni ukiwa.^b

27 “Naye atalitendesha agano kwa ajili ya wengi kwa juma moja; na katika nusu ya juma hilo atakomesha dhambi-hu na toleo la zawadi.^c

“Na juu ya bawa la vitu vye-nye kuchukiza sana kutakuwa na yule anayesababisha ukiwa;^d na mpaka wakati wa maangamizi, kilichoamuliwa kitamwagwa pia juu ya yule anayekaa ukiwa.”

10 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Koroshi^e mfalme wa Uajemi, Danieli ambaye pia aliitwa Belteshaza^f alipewa ufunuo; na ujumbe wake ulikuwa wa kweli, nao ulihusu pambano kubwa. Naye alielewa ujumbe huo na kupewa uelewaji kuhusu mambo aliyokuwa ameona.

2 Siku hizo, mimi, Danieli, nilikuwa nikiomboleza^g kwa majuma matatu kamili. **3** Sikula kamwe chakula kizuri, sikula nyama wala kunywa divai, nami sikujipaka kamwe mafuta kwa majuma matatu kamili. **4** Katika siku ya 24 ya mwezi wa kwanza, nilipokuwa kwenye ukingo wa ule mto mkubwa, Mto Tigri,^{*h} 5 nili-nua macho yangu nikamwona mwanamume aliyevaa mavazi ya kitani,ⁱ na kiunoni mwake alikuwa na mshipi wa dhahabu kutoka Ufazi. **6** Mwili wake ulikuwa kama krisolito,^j uso wake ulionekana kama radi, macho yake yalikuwa kama mienge inayowaka moto, mikono yake na miguu yake ilio-

10:4 *Tnn., “Hidekeli.”

SURA YA 9

a Mt 24:15
Lu 19:43, 44
Lu 21:20

b Lu 21:22, 24

c Ebr 9:11, 12
Ebr 10:8-10

d Mk 13:14
Lu 21:20

SURA YA 10

e Ebr 1:1, 2
Isa 45:1
Da 1:21
Da 6:28

f Da 1:7
Da 4:8

g Da 9:3

h Mwa 2:14

i Ufu 19:14

j Eze 1:16

Safu ya 2

a Eze 1:5, 7

b 2Fa 6:17
Mdo 9:7

c Da 7:28
Da 8:27

d Da 8:18

e Yer 1:9
Ufu 1:17

f Da 9:23
Da 10:19

g Ufu 1:17

h Da 9:23

i Efe 6:12

j Da 10:21
Da 12:1
Yud 9
Ufu 12:7, 8

nekana kama shaba iliyong’arishwa,^a na mvumo wa maneno yake ulikuwa kama mvumo wa umati wa watu. **7** Ni mimi Danieli, peke yangu, niliyeona maono hayo; wanaume waliokuwa pamoja nami hawakuyaona.^b Hata hivyo, walishikwa na hofu kubwa, wakakimbia na kujificha.

8 Kisha nikabaki peke yangu, na nilipoona maono hayo makubwa nguvu ziliniishia na sura yangu ya heshima ikatoweka, nikapoteza nguvu zote.^c **9** Kisha nikasikia sauti yake akizungumza; lakini nilipomsikia akizungumza, nikalala kifudufudi ardhini na kushikwa na usingizi mzito.^d **10** Lakini mkono ukani-gusa,^e ukanitikisa ili niinuke kwa mikono na magoti yangu. **11** Kisha akaniambia:

“Ee Danieli, wewe mtu mwenye thamani sana,^{*f} sikiliza kwa makini maneno ninayotaka kukwambia. Sasa simama mahali ulipo, kwa maana ni-metumwa kwako.”

Aliponiambia maneno hayo, nikasimama nikitetemeka.

12 Kisha akaniambia: “Usiogope,^g Ee Danieli. Maneno yako yamesikiwa tangu siku ya kwanza ulipoukaza moyo wako kupata uelewaji na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, nami nimekuja kwa sababu ya maneno yako.^h

13 Lakini mkuuⁱ wa ufalme wa Uajemi alinipinga kwa siku 21. Lakini Mikaeli,^{*j} mmoja wa wakuu wenye vyeo vya juu zaidi,[#] akaja kunisaidia; nami

10:11 *Au “anayependwa sana; anayeheshimiwa sana.” 10:13 *Maana yake “Ni Nani Aliye Kama Mungu?” #Au “mkuu wa cheo cha kwanza.”

nikabaki huko kando ya wafalme wa Uajemi. **14** Nimekuja kukueleweshwa mambo yatakayowapata watu wako katika kipindi cha mwisho cha zile siku,^a kwa maana ni maono yanayohusu siku zijazo.”^b

15 Sasa aliponiambia maneno hayo, niliuiamisha uso wangu chini nikashindwa kungea. **16** Ndipo mmoja aliyeonekana kama mwanadamu akaigusa midomo yangu,^c nami nikafungua kinywa changu na kumwambia yule aliyesimama mbele yangu: “Bwana wangu ninaogopa kwa sababu ya maono hayo, nami sina nguvu.”^d **17** Sasa bwana wangu, mimi mtumishi wako, ninawezaje kuzungumza nawe bwana wangu?^e Kwa maana sasa sina nguvu, na pumzi imeniishia.”^f

18 Yule aliyeonekana kama mwanadamu akanigusa tena na kunitia nguvu.^g **19** Kisha akasema: “Usiogope,^h Ee mtu mwenye thamani sana.*ⁱ Uwe na amani.^j Uwe na nguvu, naam, uwe na nguvu.” Alipokuwa akizungumza nami nilitiwa nguvu na kusema: “Bwana wangu, sema, kwa maana umenitia nguvu.”

20 Ndipo akasema: “Je, unajua kwa nini nimekuja? Sasa nitarudi kupigana na mkuu wa Uajemi.^k Nitakapoondoka, mkuu wa Ugiriki atakuja. **21** Hata hivyo, nitakwambia mambo yaliyoandikwa katika kitabu cha kweli. Hakuna yeyote anayeniunga mkono kwa uthabiti katika mambo haya isipokuwa Mikaeli,^l mkuu wako.”^m

10:19 *Au “anayependwa sana; anayeheshimiwa sana.”

SURA YA 10

a Da 2:28

b Da 8:17, 26
Da 12:4c Isa 6:7
Yer 1:9

d Da 10:8

e Amu 6:22

f Isa 6:5

g Da 10:10

h Ufu 1:17

i Da 9:22, 23
Da 10:11

j Amu 6:23

k Da 10:13

l Da 10:13
Yud 9
Ufu 12:7, 8

m Da 12:1

Safu ya 2

SURA YA 11

a Da 5:30, 31
Da 9:1

b Da 8:21

c Da 8:5, 21

d Da 7:6
Da 8:8, 22

11 “Mimi, katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Dario^a Mmedi, nilisimama ili kumtia nguvu na kumwimarisha.* **2** Nitakayokwambia sasa ndiyo kweli:

“Tazama! Wafalme watatu zaidi watasimama* kwa ajili ya Uajemi, na wa nne atajikusanyia utajiri mwingi zaidi kuliko wengine wote. Na atakapokuwa na nguvu kupitia utajiri wake, atachochea kila kitu dhidi ya ufalme wa Ugiriki.^b

3 “Na mfalme mwenye nguvu atasimama na kutawala kwa mamlaka kubwa sana^c na kufanya apendavyo. **4** Na atakapokuwa amesimama, ufalme wake utavunjwa na kugawanywa kuelekea pepo nne za mbinguni,^d lakini si kwa wazao wake* na si kwa mamlaka aliyotawala nayo; kwa maana ufalme wake utang’olewa na kuchukuliwa na wengine zaidi ya hao.

5 “Na mfalme wa kusini atakuwa na nguvu, yaani, mmoja wa wakuu wake; lakini kuna mmoja atakayemshinda na kutawala kwa mamlaka kubwa sana, kubwa kuliko mamlaka yake.

6 “Baada ya miaka kadhaa wataungana, na binti ya mfalme wa kusini atakuja kwa mfalme wa kaskazini ili kufanya makubaliano. Lakini nguvu za mkono wa binti huyo hazitadumu; na mfalme huyo hatasimama, wala mkono wake; na binti huyo atatiwa mikononi mwa wengine, yeye pamoja na wale wanaomleta, na yule aliyemzaa, na yule

11:1 *Au “kuwa kama ngome kwake.”

11:2 *Au “watainuka.” **11:4** *Au “kizazi chake kijacho.”

atakayemtia nguvu nyakati hizo. **7** Na mmoja kutoka katika chipukizi la mizizi yake atasimama katika cheo cha mfalme huyo, na mfalme huyo atalijia jeshi na kushambulia ngome ya mfalme wa kaskazini naye atachukua hatua dhidi yao na kushinda. **8** Mfalme huyo atakuja Misri pamoja na miungu yao, sanamu zao za chuma,* na vitu vyao vinavyotamanika# vya fedha na vya dhahabu, pamoja na mateka. Kwa miaka kadhaa hatamshambulia mfalme wa kaskazini, **9** ambaye atashambulia ufalme wa mfalme wa kusini, lakini atarudi katika nchi yake mwenyewe.

10 "Na wanawe watajitayarisha kwa ajili ya vita na kukusanya jeshi kubwa sana. Naye hakika atasonga mbele na kupita kama mafuriko. Lakini atarudi, naye atapigana vita mpaka kwenye ngome yake.

11 "Na mfalme wa kusini atakasirika, naye atatoka na kwenda kupigana naye, yaani, na mfalme wa kaskazini, ambaye atakusanya umati mkubwa wa watu, lakini umati huo utatiwa mikononi mwa mfalme huyo.* **12** Na umati huo utachukuliwa. Moyo wake utajikweza, naye atasababisha makumi ya maelfu wanguke; lakini hatatumia nafasi aliyopata ya ushindi.

13 "Na mfalme wa kaskazini atarudi na kukusanya umati mkubwa zaidi kuliko ule wa kwanza; na mwishoni mwa zile nyakati, baada ya miaka ka-

11:8 *Au "sanamu zao za kuyeyushwa."
#Au "vyenye thamani." 11:11 *Inaonekana ni mfalme wa kusini.

Safu ya 2

SURA YA 11

a Zb 48:2
Da 8:9
Da 11:41, 45

dhaa, kwa hakika atakuja na jeshi kubwa na mali nyingi. **14** Nyakati hizo wengi watampinga mfalme wa kusini.

"Na watu wakatili* miongoni mwa watu wako watashawishiwa kujaribu kutimiza maono; lakini watajikwaa.

15 "Na mfalme wa kaskazini atakuja na kujenga boma la kuzingira na kuteka jiji lenye ngome. Na majeshi ya kusini hayatasimama,* wala wanaueme wake mashujaa; nao hawatakuwa na nguvu za kusimama. **16** Yule anayekuja kupigana naye atafanya apendavyo, na hakuna yeyote atakayesimama mbele yake. Atasimama katika nchi ya lile Pambbo,*^a na uwezo wa kuangamiza utakuwa mikononi mwake. **17** Naye ataaizimia kabisa* kuja na nguvu kamili za ufalme wake, atafanya makubaliano pamoja na mfalme huyo; naye atatenda kwa mafanikio. Na kumhusu yule binti wa wanawake, mfalme huyo atapewa ruhusa ya kumwangamiza. Na binti huyo hatasimama, wala hataendelea kuwa wake. **18** Mfalme huyo ataugeza uso wake na kurudi kwenye nchi za pwani, naye atateka maeneo mengi. Na kamanda fulani atakomesha kwa faida yake mwenyewe ufidhuli kutoka kwa mfalme huyo, hivi kwamba ufidhuli huo hautakuwepo. Ataufanya umrudie mfalme huyo. **19** Kisha* ataugeza

11:14 *Au "wana wa wanyang'anyi."

11:15 *Tnn., "mikono ya kusini hatasimama." 11:16 *Au "ule Urembo."

11:17 *Tnn., "atakaza uso wake kabisa."

11:19 *Inaonekana ni mfalme wa kaskazini.

uso wake kurudi kwenye ngome za nchi yake mwenyewe, naye atajikwaa na kuanzuka, na hatapatikana.

20 "Na katika cheo chake atasimama mtu anayemfanya mtozaji* apite katika ufalme wenye fahari, lakini katika siku chache atavunjwa, ingawa si kwa hasira wala vitani.

21 "Na katika cheo chake atasimama mtu anayedharauliwa,* nao hawatampa fahari ya ufalme huo; naye atakuja wakati wa usalama[#] na kuchukua ufalme kwa ujanja.^Δ

22 Na majeshi yaliyo kama mafuriko yatafagiliwa* mbali kwa sababu yake, nayo yataangamizwa; kama itakavyokuwa kwa Kiongozi^a wa lile agano.^b

23 Na kwa sababu ya muungano waliofanya naye, ataendeleza udanganyifu na kuinuka na kuwa mwenye nguvu kupitia taifa dogo. **24** Wakati wa usalama,* atavamia maeneo ya mkoa[#] yenye utajiri mwingi zaidi^Δ na kufanya mambo ambayo baba zake na mababu zake hawakufanya. Atawagawia watu wake vitu alivyopora na nyara na mali; naye atapanga njama zake dhidi ya mahali penye ngome, lakini kwa muda tu.

25 "Akiwa na jeshi kubwa, atakusanya nguvu zake na moyo wake dhidi ya mfalme wa kusini atajitayarisha kwa ajili ya vita hivyo akiwa na jeshi ku-

11:20 *Huenda ni "mtoza ushuru." Au "msimamizi wa kazi." 11:21 *Au "anayechukiza." [#]Au labda, "bila onyo." ^ΔAu "hila." 11:22 *Tnn., "mikono ya mafuriko itafagiliwa." 11:24 *Au labda, "Bila onyo." [#]Au "wilaya ya utawala." ^ΔTnn., "unono."

SURA YA 11

a Da 9:25
Yoh 1:45, 49

b Mwa 15:18
Mdo 3:25

Safu ya 2

a Da 12:9

b Mwa 10:4
Hes 24:24
Isa 23:1
Yer 2:10
Eze 27:6

c Da 11:28

d Da 8:11

e Da 8:12

f Da 12:11
Mt 24:15
Mk 13:14
Lu 21:20

bwa kupita kiasi, tena lenye nguvu. Naye hatasimama, kwa sababu watapanga njama dhidi yake. **26** Na wale wanaokula vyakula vyake bora wata-sababisha aanguke.

"Na jeshi lake litafagiliwa mbali, na wengi watauawa.

27 "Kuhusu wafalme hawa wawili, moyo wao utakuwa na mwelekeo wa kufanya mauvu, nao wataketi kwenye meza moja wakiambiana uwongo. Lakini hakuna lolote litakalofanikiwa, kwa maana mwisho utakuja kwa wakati ulio-wekwa.^a

28 "Na mfalme wa kaskazini atarudi katika nchi yake akiwa na mali nyingi, na moyo wake utapinga lile agano takatifu. Atatenda kwa mafanikio na kurudi katika nchi yake.

29 "Kwa wakati ulioyekwa atarudi na kushambulia kusini. Lakini wakati huo mambo hayatakuwa kama yalivyokuwa mwanzoni, **30** kwa maana meli za Kitimu^b zitamshambulia, naye atanyenye-kezwa.

"Atarudi na kumwaga shutuma* dhidi ya lile agano takatifu,^c naye atatenda kwa mafanikio; atarudi na kuwakazia fikira wale wanaoliacha agano takatifu. **31** Na majeshi yatasimama, kutoka kwake; nayo yatachafua patakatifu,^d ile ngome, na kuondoa ile dhambi inayotolewa daima.^{*e}

"Nao watasimamisha kile kitu chenye kuchukiza sana kinachosababisha ukiwa.^f

32 "Na wale wanaotenda uovu dhidi ya lile agano, ata-

11:30 *Au "kuelekeza ghadhabu yake." 11:31 *Au "kile kitu kinachotolewa kila siku."

waongoza kwa maneno ya ujanja* waingie katika uasi imani. Lakini watu wanaomjua Mungu wao watakuwa imara na kutenda kwa mafanikio. **33** Na wale walio na ufahamu^a miongoni mwa watu watawasaidia wengi kupata uelewaji. Nao* watakwazwa kwa upanga na kwa mwali wa moto, kwa kutekwa na kwa kuporwa, kwa siku kadhaa. **34** Lakini watakapokwazwa, watapokea msaada kidogo; na wengi watajiunga nao kwa maneno ya ujanja.* **35** Na baadhi ya wale wenye ufahamu watakwazwa, ili kazi ya kuwasafisha watu ifanywe kwa sababu yao na kazi ya kuwatakasa na kuwafanya kuwa weupe^b mpaka wakati wa mwisho; kwa maana bado ni ya wakati uliowekwa.

36 "Mfalme huyo atafanya apendavyo, naye atajikweza na kujitukuza juu ya kila mungu; naye atasema mambo ya kushangaza dhidi ya Mungu wa miungu.^c Naye atafanikiwa mpaka shutuma itakapofikia mwisho; kwa sababu kilichoamuliwa lazima kitendeke. **37** Hatamjali Mungu wa baba zake; wala hatajali tamaa ya wanawake wala hatajali mungu mwingine yeyote, lakini atajitukuza mwenyewe juu ya kila mtu. **38** Badala ya Mungu wa baba zake atampa utukufu mungu wa ngome; na kwa kutumia dhahabu na fedha na mawe yenye thamani na vitu vinavyotamanika,* atampa utukufu mungu ambaye baba zake hawa-

11:32, 34 *Au "kurairai; yasiyo ya unyoofu." 11:33 *Yaani, walio na ufahamu. 11:38, 43 *Au "vyenye thamani."

SURA YA 11

a Da 12:10

b Da 12:10

C Kum 10:17
Zb 136:1, 2

Safu ya 2

a Zb 48:2

Da 8:9

Da 11:16, 45

b Zb 48:2

Da 8:9

Da 11:16, 41

kumjua. **39** Naye atashinda ngome zilizoimarishwa kabisa akiwa pamoja na* mungu wa kigeni. Atawapa utukufu mwingi wale wanaomtambua,[#] naye atawafanya wawatawale watu wengi; na ataigawa ardhi kwa malipo.

40 "Wakati wa mwisho mfalme wa kusini atasukumana* naye, na mfalme wa kaskazini atamshambulia vikali kwa kutumia magari ya vita na wapanda farasi na meli nyingi; naye ataingia katika nchi hizo na kupita humo kama mafuriko. **41** Ataingia pia katika nchi ya lile Pambo,^{*a} na nchi nyingi zitakwazwa. Lakini hizi ndizo nchi zitakazoponyoka mikononi mwake: Edomu na Moabu na sehemu kuu ya Waamoni. **42** Naye ataelelea kuunyoosha mkono wake kwa nguvu dhidi ya nchi hizo; na nchi ya Misri haitaponyoka. **43** Naye atawala hazina zilizofichwa za dhahabu na fedha na vitu vyote vinavyotamanika* vya Misri. Na Walibya na Waethiopia watafuata nyayo zake.[#]

44 "Lakini habari kutoka mashariki* na kutoka kaskazini zitamhangaisha, naye atatokwa kwa hasira kali ili kuwaangamiza na kuwaua wengi. **45** Naye atapiga mahema yake ya kifalme[#] kati ya bahari kuu na mlima mtakatifu wa lile Pambo;^{*b} naye atasonga kufikia mwisho wake, na hakuna atakayemsaidia.

11:39 *Au "akisaidiwa na." #Au labda, "Atampa utukufu mwingi yeyote anayemtambua." 11:40 *Au "atamenyana." 11:41, 45 *Au "ule Urembo." 11:43 *Au "watamfuata." 11:44 *Au "mawio ya jua." 11:45 *Au "ya kifahari."

12 “Wakati huo Mikaeli*^a atasimama,[#] yule mkuu^b anayesimama kwa ajili ya watu wako.[^] Na kutakuwa na wakati wa taabu ambao haujawahi kamwe kutokea tangu kuanzishwa kwa taifa lolote mpaka wakati huo. Na wakati huo watu wako wataponyoka,^c kila mtu atakayepatikana ameandikwa katika kile kitabu.^d **2** Na wengi kati ya wale wanaolala usingizi katika mavumbi ya dunia wataamka, baadhi yao watapata uzima wa milele na wengine watapata shutuma na chuki ya milele.

3 “Na wale walio na ufahamu watang’aa sana kama anga la mbingu, na wale wanaowalita wengi kwenye uadilifu watang’aa kama nyota, milele na milele.

4 “Lakini wewe, Danieli, ya-weke siri maneno haya, na ukifunge kwa muhuri kitabu hiki mpaka wakati wa mwisho.^e Wengi watazunguka huku na huku,^{*} na ujuzi wa kweli utakuwa mwingi.”^f

5 Kisha mimi, Danieli, nika-tazama na kuwaona wengine wawili wamesimama mahali hapo, mmoja kwenye ukingo huu wa kijito na yule mwingine kwenye ukingo wa pili wa kijito.^g **6** Kisha mmoja akamuuliza yule mwanamume aliyevaa mavazi ya kitani,^h aliyekuwa juu ya maji ya kijito: “Itachukua muda gani kufikia mwisho wa mambo haya ya kustaajabisha?” **7** Kisha nikamsikia yule mwanamume aliyevaa mavazi ya kitani, ali-

12:1 *Maana yake “Ni Nani Aliye Kama Mungu?” #Au “atainuka.” ^Tnn., “wana wa watu wako.” 12:4 *Au “watakichunguza [yaani, kitabu hiki] kwa makini.”

SURA YA 12

a Da 10:13
Yud 9
Ufu 12:7, 8

b Da 10:21

c Isa 26:20
Yoe 2:31, 32
Mt 24:21, 22
Ufu 7:13, 14

d Mal 3:16
Lu 10:20
Ufu 3:5

e Da 8:17, 26
Da 12:9

f Isa 11:9

g Da 10:4

h Da 10:5, 6

Safu ya 2

a Da 4:34
Ufu 4:9
Ufu 10:6

b Da 8:24

c Lu 18:34
Mdo 1:7
1Pe 1:10, 11

d Da 8:17, 26
Da 10:14
Da 12:4

e Da 11:35

f Zb 111:10
Da 11:33
Da 12:3

g Da 8:11

h Da 11:31
Mk 13:14

i Yoh 11:24
Mdo 17:31
Mdo 24:15
Ufu 20:12

yekuwa juu ya maji ya kiji-to, alipokuwa akiinua mkono wake wa kulia na mkono wake wa kushoto kuelekea mbinguni na kuapa hivi kwa jina la Yule anayeishi milele:^a “Itakuwa ni kwa wakati uliowe-kwa, nyakati zilizowekwa, na nusu ya wakati.* Mara tu kuvunjwavunjwa kwa nguvu za watu watakatifu kutakapofikia mwisho,^b mambo haya yote yatafikia mwisho wake.”

8 Basi mimi, nilisikia, lakini sikuweza kuelewa;^c kwa hiyo nikauliza: “Ee bwana wangu, matokeo ya mambo haya yote yatakuwa nini?”

9 Akajibu: “Nenda, Danieli, kwa sababu maneno haya yanapaswa kuwekwa yakiwa siri na kutiwa muhuri mpaka wakati wa mwisho.^d **10** Wengi watajitakasa na kujifanya weupe nao watasafishwa.^e Na waovu watatenda uovu, na hakuna mwovu yeyote atakayeelewa; lakini wale walio na ufahamu wataelewa.^f

11 “Na tangu wakati wa kuondolewa kwa ile dhabihu inayotolewa daima*^g na kusi-mamishwa kwa kile kitu kinachochukiza sana kinachosababisha ukiwa,^h kutakuwa na siku 1,290.

12 “Mwenye furaha ni yule anayeendelea kutarajia* na anayefika kwenye zile siku 1,335!

13 “Lakini wewe, endelea mpaka mwisho. Utapumzika, lakini utasimama kwa ajili ya fungu lako* mwishoni mwa zile siku.”ⁱ

12:7 *Yaani, nyakati tatu na nusu. 12:11 *Au “kile kitu kinachotolewa kila siku.” 12:12 *Au “anayengojea kwa hamu kubwa.” 12:13 *Au “mahali pako ulipogawiwa.”

HOSEA

YALIYOMO

- | | |
|---|--|
| <p>1 Mke wa Hosea na watoto anaozaa (1-9)
Yezreeli (4), Lo-ruhama (6), na
Lo-ami (9)
Tumaini la kurudishwa na kuwa na
umoja (10, 11)</p> <p>2 Waisraeli wasio waaminifu
waadhibiwa (1-13)
Wamrudia Yehova akiwa kama mume
wao (14-23)
"Utaniita mume Wangu" (16)</p> <p>3 Hosea amkomboa mke wake mzinzi (1-3)
Waisraeli watamrudia Yehova (4, 5)</p> <p>4 Kesi ya Yehova dhidi ya Waisraeli (1-8)
Watu hawamjui Mungu nchini (1)
Waisraeli waabudu sanamu na kufanya
ukahaba (9-19)
Wapotoshwa na roho ya ukahaba (12)</p> <p>5 Waefraimu na watu wa Yuda
wahukumiwa (1-15)</p> <p>6 Wasihiwa wamrudie Yehova (1-3)
Upendo mshikamanifu usiodumu wa
Waisraeli (4-6)
Upendo mshikamanifu ni bora kuliko
dhabihu (6)
Mwenendo wa aibu wa Waisraeli (7-11)</p> <p>7 Uovu wa Waefraimu (1-16)
Hawataepuka wavu wa Mungu (12)</p> <p>8 Matokeo ya kuabudu sanamu (1-14)</p> | <p>Kupanda upepo, kuvuna
kimbunga (7)
Waisraeli wamemsahau Muumba
wao (14)</p> <p>9 Mungu awakataa Waefraimu kwa
sababu ya dhambi zao (1-17)
Wajiweka wakfu kwa mungu
anayechukiza (10)</p> <p>10 Waisraeli ni mzabibu ulioharibika,
wataangamizwa (1-15)
Kupanda na kuvuna (12, 13)</p> <p>11 Mungu ampenda Israeli tangu
utotoni (1-12)
"Nikamwita mwanangu atoke
Misri" (1)</p> <p>12 Waefraimu wanapaswa kumrudia
Yehova (1-14)
Yakobo alishindana na Mungu (3)
Yakobo alimlilia Mungu ili
ambariki (4)</p> <p>13 Waefraimu waabudu sanamu na
kumsahau Yehova (1-16)
"Ewe Kifo, yako wapi maumivu yako
makali?" (14)</p> <p>14 Wasihiwa wamrudie Yehova (1-3)
Kutoa sifa ya midomo (2)
Waisraeli waponywa, hawatakosha
uaminifu tena (4-9)</p> |
|---|--|

1 Neno la Yehova lililomjia Hosea* mwana wa Beer katika siku za Uzia,^a Yothamu,^b Ahazi,^c na Hezekia,^d walalimwa na Yuda,^e na katika siku za Yeroboamu^f mwana wa Yoashi,^g mfalme wa Israeli. **2** Yehova alipoanza kusema neno lake kupitia Hosea, Yehova

1:1 *Ufupisho wa jina Hoshaya, linaloamaanisha "Aliyeokolewa na Yah; Yah Ameokoa."

SURA YA 1

a 2Nya 26:1, 3, 4

b 2Fa 15:32-34

c 2Fa 16:1-3

d 2Fa 18:1-3

e Isa 1:1

Mik 1:1

f 2Fa 14:23, 24

Amo 1:1

g 2Fa 13:10, 11

Safu ya 2

a Kum 31:16

Ho 3:1

alimwambia hivi Hosea: "Nenda, muoe mwanamke kaha-ba* na uzae watoto wa ukahaba,"^a kwa sababu nchi imeacha kabisa kumfuata Yehova kwa sababu ya ukahaba."^a

3 Basi akaenda na kumwoa Gomeri binti ya Diblaimu, na Gomeri akapata mimba na kumzalima mwana.

1:2 *Au "malaya." ^aAu "umalaya."

4 Kisha Yehova akamwambia Hosea: "Mpe mwana huyo jina Yezreeli,* kwa sababu baada ya muda mfupi tu nitaifanya nyumba ya Yehu^a iwajibike kwa sababu ya matendo ya umwagaji wa damu ya Yezreeli, nami nitaukomesha utawala wa wafalme wa Israeli.^b 5 Siku hiyo nitavunja upinde wa Israeli katika Bonde la* Yezreeli."

6 Gomeri akapata mimba tena na kuzaa binti. Mungu akamwambia Hosea: "Mpe binti huyo jina Lo-ruhama,* kwa maana sitaionyesha tena rehema^c nyumba ya Israeli, kwa sababu kwa hakika nitawafukuza.^d 7 Lakini nitaionyesha rehema nyumba ya Yuda,^e nami nitawaokoa kwa nguvu za Yehova Mungu wao;^f sitawaokoa kwa upinde au kwa upanga au kwa vita au kwa farasi au kwa wapanda farasi."^g

8 Baada ya kumwachisha Lo-ruhama kunyonya, Gomeri alipata mimba na kuzaa mwana. 9 Kisha Mungu akasema: "Mpe mwana huyo jina Lo-ami,* kwa sababu ninyi si watu wangu nami sitakuwa Mungu wenu.

10 "Na Waisraeli* watakuwa wengi kama chembe za mchanga wa bahari, ambao hauwezi kupimwa wala kuhesabiwa.^h Na mahali ambapo Mungu aliwaambia, 'Ninyi si watu wangu,'ⁱ atawaita, 'Wana wa Mungu aliye hai.'^j 11 Na watu wa Yuda na wa Israeli watakusanywa pamoja

1:4 *Maana yake "Mungu Atapanda Mbegu." 1:5 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya." 1:6 *Maana yake "Hajaonyeshwa Rehema." 1:9 *Maana yake "Si Watu Wangu." 1:10 *Yaani, wana wa Israeli.

SURA YA 1

a 2Fa 10:29-31

b 2Fa 15:8, 10

c Ho 2:23

d 2Fa 17:6
2Fa 17:22, 23

e Ho 11:12

f 2Fa 19:34, 35

g Isa 37:36

h Mwa 13:16
Mwa 22:17

i 1Pe 2:10

j Ro 9:25, 26
2Ko 6:18

Safu ya 2

a Ezz 3:1
Isa 11:12
Yer 3:18
Eze 37:19
Mik 2:12

b Ho 2:22

SURA YA 2

c Yer 31:33
Eze 36:28
Zek 13:9

d Ho 2:23

e Yer 3:8

f Eze 23:4, 5
Ho 3:1g Ezz 9:6
Da 9:7
Ho 9:10h Eze 23:7, 8
Ho 8:9

ili wawe na umoja^a nao watajichagulia kiongozi mmoja na kupanda kutoka nchini, kwa maana siku ya Yezreeli itakuwa kuu.^b

2 "Waambieni ndugu zenu, 'Ninyi ni watu wangu!'^{*c}

Na dada zenu, 'Enyi wana-wake mlioonyesha rehema!'^{#d}

2 Mshtakini mama yenu; mshtakini,

Kwa maana yeye si mke wangu^e nami si mume wake.

Anapaswa kuacha ukahaba*^f

Na uzinzi kutoka kati ya matiti yake,

3 La sivyo nitamvua nguo abaki uchi kama alivyo-zaliwa,

Nitamfanya awe kama nyika,

Nitamfanya awe nchi isiyoni maji,

Na kusababisha afe kwa kiu.

4 Nami sitawaonyesha rehema wanawe,

Kwa maana ni wana wa ukahaba.*^g

5 Kwa maana mama yao amefanya ukahaba.*^f

Aliyewachukua mimba ametenda kwa aibu,^g

kwa kuwa alisema, 'Nitawafuatia wapenzi wangu,^h

Wanaonipa mkate wangu[#] na maji yangu,

Sufu yangu na kitani changu, mafuta yangu na kinnywaji changu.'

2:1 *Angalia maelezo ya chini ya Hosea 1:9. #Angalia maelezo ya chini ya Hosea 1:6. 2:2, 4, 5 *Au "umalaya." 2:5 *Au "chakula changu."

- 6** Basi nitaziba njia yako kwa uzio wa miiba; Nami nitajenga ukuta wa mawe ili kumzuia, Ili asiweze kupata njia za kutokea.
- 7** Atawafuatia wapenzi wake, lakini hatawapata;^a Atawatafuta, lakini hatawapata. Kisha atasema, 'Nitarudi kwa mume wangu wa kwanza,^b Kwa maana nilikuwa na hali njema zaidi wakati huo kuliko sasa.'^c
- 8** Hakutambua kwamba mimi ndiye niliyempa nafaka,^d divai mpya, na mafuta, Na mimi ndiye niliyempa fedha nyingi Na dhahabu, waliyotumia kumtumikia Baali.^e
- 9** 'Kwa hiyo, nitarudi na kuchukua nafaka yangu ita- kapokomaa Na divai yangu mpya kati- ka majira yake,^f Nami nitampokonya sufu yangu na kitani changu kilichokusudiwa kufuni- ka uchi wake.
- 10** Naam, nitafunua sehemu zake za siri ili wapenzi wake wazione waziwazi, Na hakuna mtu yeyote atakayemwokoia kutoka mi- kononi mwangu.^g
- 11** Nitakomesha shangwe yake yote, Sherehe zake,^h miezi yake mipya, sabato zake, na misimu yake yote ya she- rehe.
- 12** Nami nitaharibu mizabibu yake na mitini yake,

SURA YA 2

a Isa 31:1
Ho 5:13

b Yer 31:18
Eze 23:4
Ho 5:15

c Kum 32:12-14
Ne 9:25

d Kum 32:28
Isa 1:3

e Ho 8:4

f Isa 17:11

g Zb 50:22
Ho 5:14

h Amo 5:21
Amo 8:10

Safu ya 2

a Amu 3:7
1Fa 16:30-32
2Fa 10:28
Ho 11:2

b Isa 17:10

c Kum 30:5
Isa 65:21
Yer 32:15
Eze 28:25, 26
Amo 9:14

d Yos 7:24-26
Isa 65:10

e Kut 15:1

f Kut 23:13
Yos 23:6, 7

g Zek 13:2

h Eze 34:25

ambayo amesema hivi kuihusu:

"Haya ni malipo yangu, ni- liyopewa na wapenzi wa- ngu";

Nitaifanya iwe misitu, Na wanyama wa mwituni wataila kwa pupa.

13 Nitamfanya awajibike kwa sababu ya siku alizotu- mia kutoa dhabihu kwa sanamu za Baali,^a

Alipokuwa akijipamba kwa pete zake na mapa- mbo yake na kuwafuatia wapenzi wake,

Na mimi ndiye aliyenisa- hau,^b asema Yehova.

14 'Kwa hiyo nitamshawishi, Nitampeleka nyikani, Nami nitazungumza naye ili kuuteka moyo wake.

15 Nitamrudishia mashamba yake ya mizabibu kua- nzia wakati huo na kue- ndelea,^c

Na Bonde la* Akori^d liwe lango la tumaini;

Atanijibu huko kama alivyofanya alipokuwa kijana,

Kama siku aliyotoka kati- ka nchi ya Misri.^e

16 Na siku hiyo,' asema Ye- hova, 'Utaniita mume Wangu, hutaniita tena bwana Wangu.'^f

17 'Nitaondoa majina ya sa- namu za Baali katika ki- nywa chake,^f

Na majina yake hayataku- mbukwa tena.^g

18 Siku hiyo nitafanya agano na wanyama wa mwituni kwa ajili ya watu wangu,^h

2:15 * Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

2:16 * Au "Baali Wangu."

Pia na ndege wa angani na viumbe wa ardhini wa-naotambaa;^a

Nitaondoa upinde na upanga na vita nchini,^b

Nami nitawafanya walale* kwa usalama.^c

19 Nitakuchumbia ili uwe wangu milele;
Nitakuchumbia kwa uadilifu na kwa haki,
Kwa upendo mshikamani-fu na kwa rehema.^d

20 Nitakuchumbia kwa uaminifu,
Nawe hakika utanijua mimi, Yehova.^e

21 'Siku hiyo nitajibu,' asema Yehova,
'Nitazijibu mbingu,
Nazo zitajibu dunia;^f

22 Nayo dunia itajibu nafaka na divai mpya na mafuta;
Navyo vitajibu Yezreeli.*^g

23 Nitampanda kama mbegu kwa ajili yangu duniani,^h
Nami nitamwonyesha rehema yule ambaye ha-kuonyeshwa rehema;*
Nitawaambia wale ambao si watu wangu:# "Ninyi ni watu wangu,"ⁱ
Nao watasema: "Wewe ni Mungu wetu.""^j

3 Kisha Yehova akania-ambia: "Nenda tena, mpende mwanamke anayependwa na mwanamume mwingine na ambaye anafanya uzinzi,^k mpende kama Yehova anavyowapenda Waisraeli^l ingawa wanaabudu miungu mingine^m

2:18 *Au "waishi." 2:22 *Maana yake "Mungu Atapanda Mbegu." 2:23 *Angalia maelezo ya chini ya Hosea 1:6. #Angalia maelezo ya chini ya Hosea 1:9.

SURA YA 2
a Isa 11:6-8

b Isa 2:4
Eze 39:9
Zek 9:10

c Law 26:5, 6
Yer 23:6
Mik 4:3, 4

d Mik 7:18

e Isa 54:13
Yer 24:7
Yer 31:34

f Kum 28:12
Zek 8:12

g Ho 1:11

h Yer 31:27

i Ho 2:1
Ro 9:25, 26
1Pe 2:10

j Ho 1:10

SURA YA 3

k Ho 1:2, 3

l Kum 7:6-8
2Fa 13:23
Zb 106:44, 45

m Amu 10:13
Yer 3:20

Safu ya 2

a 2Fa 17:6
2Fa 18:9, 10

b Amu 8:27

c Amu 17:5
1Sa 19:15, 16

d Yer 50:4

e Yer 30:9
Eze 34:23, 24
Eze 37:24, 25
Amo 9:11
Lu 1:31-33

f Kum 4:30

SURA YA 4

g Mik 6:2

h Mik 7:2

i Ho 11:12

j 1Fa 21:18, 19

k Eze 23:37

l Ho 1:4
Ho 6:8, 9

m Amu 8:7, 8

na kupenda keki za zabibu kavu."*

2 Basi nikamnunua ili awe wangu kwa vipande 15 vya fedha na homeri moja na nusu* ya shayiri. **3** Kisha nikamwambia: "Utaendelea kuwa wangu kwa siku nyingi. Usifanye ukahaba,* na usifanye ngono na mwanamume mwingine, nami pia sitafanya ngono nawe."

4 Kwa maana Waisraeli watakaa kwa muda mrefu* bila mfalme,^a bila mkuu, bila dhahibu, bila nguzo, na bila efo-di^b na sanamu za terafimu."^c

5 Baadaye Waisraeli watarudi na kumtafuta Yehova Mungu wao^d na Daudi mfalme wao,^e nao watamjia Yehova wakitete-meka na kutafuta wema wake katika kipindi cha mwisho cha zile siku.^f

4 Lisikieni neno la Yehova, enyi Waisraeli,

Kwa maana Yehova ana kesi dhidi ya wakaaji wa nchi,^g

Kwa sababu hakuna ukweli wala upendo mshikamanifu wala ujuzi ku-mhusu Mungu nchini.^h

2 Viapo vya uwongo na udanganyifuⁱ na mauaji/
Na wizi na uzinzi^k umee-nea sana,

Na tendo moja la umwagaji wa damu linafuata tendo lingine la umwagaji wa damu.^l

3 Ndiyo sababu nchi itaomboleza^m

3:1 *Yaani, keki zilizotumiwa katika ibada ya uwongo. 3:2 *Homeri ni kipimo sawa na lita 220. Angalia Nyongeza B14. 3:3 *Au "umalaya." 3:4 *Tnn., "siku nyingi." #Au "miungu ya familia; sanamu."

Na kila mkaaji nchini atadhooifika;

Wanyama wa mwituni na ndege wa angani,
Hata samaki wa baharini,
wataangamia.

4 “Hata hivyo, mtu yeyote asibishane nanyi wala kuwakaripia,^a

Kwa maana watu wenu ni kama wale wanaobishana na kuhani.^b

5 Basi mtajikwaa kweupe kabisa wakati wa mchana,

Na nabii atajikwaa pamoja nanyi, kana kwamba ni usiku.

Nami nitamnyamazisha* mama yenu.

6 Watu wangu watanyamazi-shwa,* kwa sababu hawana ujuzi.

Kwa sababu mmekataa ujuzi,^c

Nitawakataa pia msinitu-mikie mkiwa makuhani wangu;

Na kwa sababu mmesahau sheria[#] ya Mungu wenu,^d

Mimi mwenyewe nitawasahau wana wenu.

7 Kadiri walivyoongezeka,* ndivyo walivyozidi kunitendea dhambi.^e

Nitabadili utukufu wao uwe aibu.[#]

8 Wanajilisha dhambi ya watu wangu,

Na wana pupa ya kuona watu wangu wakikosea.

9 Yatakayowapata watu

4:5 *Tnn., “nitamwangamiza.” 4:6 *Tnn., “wataangamizwa.” #Au “mafundisho.” 4:7 *Yaani, makuhani. #Au labda, “Wameniaibisha badala ya kunitukuza.”

SURA YA 4

a Amo 5:10,13

b Kum 17:12

c Yer 2:8

d 2Fa 17:15, 16

e Eze 9:6, 7

Safu ya 2

a Amo 3:1, 2

b Law 26:26
Mik 6:14

c Ho 9:11, 12

d Met 20:1
Met 23:31, 33
Isa 28:7

e Yer 3:6

f 2Fa 17:10-12
Yer 2:20
Eze 20:28

ndiyo yatakayompata kuhani;

Nitawafanya wawajibike kwa sababu ya njia zao, Nami nitawaletea matokeo ya matendo yao.^a

10 Watakula lakini hawata-shiba.^b

Watafanya ngono ovyovyoo,* lakini hawataongezeka,^c

Kwa sababu hawajamheshimu Yehova.

11 Ukahaba* na divai na divai mpya

Huondoa kichocheo cha kutenda lililo jema.^{#d}

12 Watu wangu hutafuta ushauri kutoka kwa sanamu zao za miti,

Wakifanya mambo wanayoambiwa na fimbo yao;*

Kwa sababu roho ya ukahaba[#] huwapotosha,

Na kwa ukahaba[#] wao wanakataa kujinyenyekeza kwa Mungu wao.

13 Wanatoa dhabihu juu ya vilele vya milima,^e

Na juu ya vilima wanafukiza moshi wa dhabihu,

Chini ya mialoni na milubna na kila mti mkubwa,^f

Kwa sababu vivuli vyake ni vizuri.

Ndiyo sababu mabinti wenu wanafanya ukahaba[#]

Na mabinti wakwe zenu wanafanya uzinzi.

14 Sitawafanya mabinti wenu

4:10 *Au “Watakuwa waasherati kupindukia; Watafanya umalaya.” 4:11 *Au “Umalaya.” #Tnn., “Huondoa moyo.” 4:12 *Au “fimbo yao ya ubashiri.” 4:12, 13 *Au “umalaya.”

- wawajibike kwa sababu ya ukahaba* wao, Wala mabinti wakwe zenu kwa sababu ya uzinzi wao. Kwa maana wanaume huwatafuta makahaba Nao hutoa dhabihu pamoja na makahaba wa heka-luni; Watu kama hao wasio na uelewaji^a wataa-ngamia.
- 15** Ingawa mnafanya ukahaba,* enyi Waisraeli,^b Watu wa Yuda wasiwe na hatia.^c Msije Gilgali^d wala Beth-aveni,^e Na msiape mkisema, 'Kwa hakika kama Yehova anavyoishi!'^f
- 16** Waisraeli wamekuwa wakaidi kama ng'ombe mkaidi.^g Je, sasa Yehova atawachunga kama mwanakondoo dume malishoni?*
- 17** Waefraimu wameshikamana na sanamu.^h Waacheni!
- 18** Pombe yao* inapomalizika, Wanafanya ngono ovyovyoo.[#] Na watawala wao[^] hupe-nda sana aibu.ⁱ
- 19** Upepo utawafunga katika mabawa yake,* Nao watazonea aibu dhabi-hu zao."

4:14, 15; 5:4 *Au "umalaya." 4:16 *Tnn., "mahali penye nafasi ya kuto-sha." 4:18 *Au "Pombe yao ya ngano." #Au "Wanafanya uasherati kupindukia; Wanafanya ukahaba." ^Tnn., "ngao zao." 4:19 *Au "utawafagilia mbali."

SURA YA 4

a Yer 4:22

b Eze 23:4, 5

c 2Fa 17:18

d Ho 9:15
Ho 12:11
Amo 4:4e Ho 5:8
Ho 10:5f Isa 48:1
Yer 5:2
Eze 20:39g Zb 78:8
Zb 81:11, 12
Zek 7:11, 12h Ho 11:2
Ho 13:1, 2

i Mik 7:3

Safu ya 2

SURA YA 5

a Ho 4:9

b Amu 4:6
Yer 46:18c Eze 23:4, 5
Ho 4:17, 18d Ho 4:12
Amo 2:7e Isa 9:9, 10
Ho 7:10f 2Fa 17:19, 20
Eze 23:30, 31
Amo 2:4, 5

- 5** "Sikieni jambo hili, enyi makuhani,^a Sikiliza kwa makini, Ee nyumba ya Israeli, Sikiliza, Ee nyumba ya mfalme, Kwa maana hukumu inawahusu ninyi; Kwa sababu ninyi ni mtego kwa Mispa Na wavu uliotandazwa juu ya Tabori.^b
- 2** Na wale wanaoanguka* wamezama ndani kabisa[#] katika mauaji, Nami ninawaonya[^] wote.
- 3** Ninawajua Waefraimu, Na Waisraeli hawajafichika mbele zangu. Kwa maana sasa, enyi Waefraimu, mmefanya ngono ovyovyoo;* Waisraeli wamejichafua wenyewe.^c
- 4** Shughuli zao haziwaruhusu wamrudie Mungu wao, Kwa sababu kuna roho ya ukahaba* miongoni mwao;^d Nao hawamtambui Yehova.
- 5** Kiburi cha Waisraeli kime-toa ushahidi dhidi yao;*^e Waisraeli na Waefraimu wamejikwaa katika kosa lao, Na watu wa Yuda wamejikwaa pamoja nao.^f
- 6** Walienda kumtafuta Yehova wakiwa na kundi lao la kondoo na kundi lao la ng'ombe,
- 5:2 *Au "waasi." #Au "wamejitumbukiza kabisa." ^Au "nitawatia nidhamu." 5:3 *Au "mmefanya uasherati; mme-fanya umalaya." 5:5 *Tnn., "mbele za uso wao."

Lakini hawakuweza kumpata.

Alikuwa amejitenga mbali nao.^a

7 Wamemsaliti Yehova,^b

Kwa sababu wamekuwa baba za wana wa kigeni.

Sasa mwezi mmoja utawanyafua* pamoja na mafungu# yao.

8 Pigeni pembe^c huko Gibeaa, tarumbeta huko Rama!^d

Pigeni kelele za vita huko Beth-aveni^e—tunawafuata, enyi Wabenjamini!

9 Enyi Waefraimu, mtakuwa kitu cha kutisha katika siku ya adhabu.^f

Nimetangaza jambo ambalo hakika litatukia miongoni mwa makabila ya Israeli.

10 Wakuu wa Yuda ni kama wale wanaosogeza mpaka.^g

Nitawamwagia ghadhabu yangu kama maji.

11 Waefraimu wamekandamiywa, wamepondwa na hukumu,

Kwa maana waliazimia kumfuata adui yao.^h

12 Kwa hiyo nilikuwa kama nondo* kwa Waefraimu Na kama uozo kwa nyumba ya Yuda.

13 Waefraimu walipoona ugonjwa wao, na watu wa Yuda kidonda chao, Waefraimu walienda Ashuruⁱ na kutuma wajumbe kwa mfalme mkuu.

Lakini hakuweza kuwaponya,

SURA YA 5

a Isa 1:15
Mik 3:4

b Isa 48:8
Yer 3:20

c Ho 8:1

d Isa 10:29

e Ho 4:15
Ho 10:5

f Isa 28:1-3
Ho 9:13

g Kum 19:14

h 1Fa 20:1

i Ho 8:9
Ho 12:1

Safu ya 2

a Zb 50:22

b Amo 2:14

c Law 26:38, 40

d Kum 4:29, 30
Kum 30:10

SURA YA 6

e Ho 5:14

Wala hakuweza kuponya kidonda chenu.

14 Kwa maana nitakuwa kama mwanasimba kwa Waefraimu, Na kama simba mwenye nguvu* kwa nyumba ya Yuda.

Mimi mwenyewe nitawarua vipandevipande na kwenda zangu;^a

Nitawabeba na kwenda nao, na hakuna yeyote atakayewaokoa.^b

15 Nitaenda na kurudi mahali pangu mpaka watakapolipia hatia yao,

Na kisha watatafuta kibali changu.*^c

Watakapokuwa wakiteseka, watanitafuta."^d

6 "Njooi, tumrudie Yehova, Kwa maana ameturarua vipandevipande,^e lakini atatuponya.

Alitupiga, lakini atafunga majeraha yetu.

2 Atatuhisha baada ya siku mbili.

Siku ya tatu atatuinua, Nasi tutaishi mbele zake.

3 Tutamjua, tutajitahidi kumjua Yehova.

Kuja kwake ni hakika kama mapambazuko; Atakuja kwetu kama mvua kubwa,

Kama mvua ya masika inayolowesha dunia."

4 "Niwafanyie nini, enyi Waefraimu?

Niwafanyie nini, enyi watu wa Yuda,

Kwa maana upendo wenu

5:7 *Au labda, "Watanyafuliwa katika mwezi mmoja." # Au "mashamba yao." 5:12 *Aina fulani ya wadudu waharibifu.

5:14 *Au "mwanasimba mwenye manyoya marefu shingoni." 5:15 *Tnn., "uso wangu."

- mshikamanifu ni kama ukungu wa asubuhi, Kama umande unaotowe-ka haraka.
- 5** Ndiyo sababu nitawakata-kata kabisa kwa kutumia manabii;^a Nitawaua kwa maneno ya kinywa changu.^b Na hukumu zangu dhidi yenu zitang'aa kama mwangaza.^c
- 6** Kwa maana ninapendezwa na upendo mshikamani-fu,^{*} si dhabihu, Na kumjua Mungu, badala ya dhabihu nzima za ku-teketezwa.^d
- 7** Lakini wao, kama wana-damu tu, wamevunja agano.^e Wamenisaliti katika nchi yao.
- 8** Gileadi ni mji wa watenda maovu,^f Umefunikwa kwa nyayo za damu.^g
- 9** Magege ya makuhani ni kama makundi ya wava-mizi yanayomvizia mtu. Wanawaua watu barabara-ni kule Shekemu,^h Kwa maana mwenendo wao ni wa aibu.
- 10** Nimeona jambo la kuchu-kiza sana katika nyumba ya Israeli. Huko Waefraimu hufanya ukahaba;ⁱ Waisraeli wamejichafua wenyewe.^j
- 11** Zaidi ya hayo, enyi watu wa Yuda, wakati wa ma-vuno umetengwa kwa ajili yenu, Nitakapowakusanya watu wangu waliotekwa."^k

6:6 *Au "rehema."

SURA YA 6

a Isa 58:1
Yer 1:9, 10
Eze 3:8, 9

b Yer 23:29

c Sef 3:5

d 1Sa 15:22
Met 21:3
Isa 1:11
Mik 6:6-8
Mt 9:13
Mt 12:7e 2Fa 17:15
Isa 24:5
Ho 8:1

f Ho 12:11

g Mik 7:2

h 1Fa 12:25

i 2Fa 17:6, 7
Yer 3:6

j Eze 23:4, 5

k Kum 30:3
Yer 29:14
Amo 9:14

Safu ya 2

SURA YA 7

a Isa 28:1

b Amo 8:14
Mik 1:5

c Mik 7:3

d Ho 6:9

e Kum 32:29
Isa 1:3
Amo 8:7f Isa 5:11
Isa 28:1

- 7** "Ninapotaka kuwaponya Waisraeli, Kosa la Waefraimu hufu-nuliwa pia,^a Na uovu wa Samaria.^b Kwa maana wamezoea udanganyifu;^c Wezi huvunja na kuingia ndani na makundi ya wa-vamizi hushambulia nje.^d
- 2** Lakini hawasemi moyoni mwao kwamba mimi ni-takumbuka uovu wao wote.^e Sasa wamezungukwa kabi-sa na shughuli zao; Ziko mbele kabisa ya uso wangu.
- 3** Wanamfanya mfalme ahangilie kwa uovu wao, Na wakuu kwa udanganyi-fu wao.
- 4** Wote ni wazinzi, Wanawaka kama jiko lili-lowashwa moto na mwo-kaji, Ambaye huacha kучо-cha moto baada ya ku-kanda unga na kuuacha uumuke.
- 5** Katika siku ya mfalme wetu, wakuu wamekuwa wagonjwa —Wana ghadhabu kwa sa-babu ya divai.^f Amewanyooshea mkono wadhhihaki.
- 6** Kwa maana wanakaribia kwa mioyo inayowaka kama jiko.^{*} Mwokaji hulala usiku kucha; Asubuhi jiko huwaka kama miali ya moto.

7:6 *Au labda, "Mioyo yao ni kama jiko wanapokaribia kwa hila."

- 7 Wote wanawaka moto kama jiko, Nao wanawanyafua watawala* wao. Wafalme wao wote wamea-nguka;^a Hakuna yeyote kati yao anayenililia.^b
- 8 Waefraimu huchangama-na na mataifa.^c Waefraimu ni kama keki ya mvingo ambayo haijao-kwa upande mmoja.
- 9 Wageni wamenyonya nguvu zao,^d lakini hawajui. Na mvi zimejaa kichwani, lakini hawana habari.
- 10 Kiburi cha Waisraeli kime-toa ushahidi dhidi yao,^e Lakini hawajamrudia Yehova Mungu wao,^f Wala hawajamtafuta licha ya hayo yote.
- 11 Waefraimu ni kama njiwa mjinga, asiye na akili.*^g Wameomba msaada Misri,^h wameenda Ashuru.ⁱ
- 12 Popote waendapo, nitatandaza wavu wangu juu yao. Nitawaangusha kama ndege wa angani. Nitawatia nidhamu kulingana na onyo ambalo kusanyiko lao lilipewa.^j
- 13 Ole wao, kwa sababu wamenikimbia! Wataangamia, kwa maana wameniasi! Nilikuwa tayari kuwakomboa, lakini wamesema uwongo dhidi yangu.^k
- 14 Hawakuniomba msaada kutoka moyoni mwao,^l Ingawa waliendelea kulia

7:7 *Tnn., "waamuzi." 7:11 *Tnn., "asiye na moyo."

SURA YA 7

a 2Fa 15:8, 10
2Fa 15:14

b Isa 9:13

c Zb 106:34-36
Eze 23:4, 5

d 2Fa 13:3
2Fa 15:19

e Ho 5:5

f Ne 9:35
Isa 9:13
Amo 4:6
Zek 1:4

g Isa 1:3

h 2Fa 15:19
Eze 23:4, 5

i 2Fa 17:4
Isa 31:1

j Kum 28:15
2Fa 17:13

k Isa 59:13

l Zb 78:37
Isa 29:13

Safu ya 2

a Zb 78:57

b Eze 36:19, 20
Ho 9:3

SURA YA 8

c Ho 5:8

d Kum 28:49, 50

e Ho 6:7

f 2Fa 17:15

g Isa 48:1
Mik 3:11

h Zb 50:17

i 1Fa 12:26, 28
Ho 13:2

j 1Fa 13:34

k Ho 10:5, 6

- kwa sauti kubwa vitandani mwao. Walijikatakata kwa sababu ya nafaka na divai yao mpya; Wananigeuka.
- 15 Ingawa niliwatia nidhamu na kuimarisha mikono yao, Wananipinga, wakipanga njama ya kutenda uovu.
- 16 Walibadili njia yao, lakini hawakufuata chochote kilichokwezwa;* Walikuwa wasiotegemeka kama upinde uliolegea.^a Wakuu wao wataangami-zwa kwa upanga kwa sababu ya ndimi zao za ukaidi. Kwa sababu hiyo watadhikiwa katika nchi ya Misri.^b
- 8 "Pigeni pembe!^c Adui anakuja kama tai kuivamia nyumba ya Yehova,^d Kwa sababu wamelivunja agano langu^e na kuasi sheria yangu.^f
- 2 Wananililia wakisema, 'Mungu wetu, sisi, Waisraeli, tunakujua!'^g
- 3 Waisraeli wamekataa mema.^h Adui na awafuatie.
- 4 Wamejichagulia wafalme, lakini bila kibali changu. Wamejichagulia wakuu, lakini sikuwatambua. Wametengeneza sanamu kwa fedha yao na dhaha-bu yao,ⁱ Wakajiletea maangamizi.^j
- 5 Ndama wenu amekataliwa, enyi watu wa Samaria.^k

7:16 *Yaani, hawakufuata ibada iliyo-kwezwa.

Hasira yangu inawaka dhidi yao.^a

Wataendelea mpaka lini kushindwa kuwa bila hatia?*

6 Kwa maana ndama huyu ametoka Israeli.

Fundi ndiye aliyemtengeneza, si Mungu;

Ndama wa Samaria atavunjwa na kubaki vipandevipande.

7 Kwa maana wanapanda upepo,

Nao watawuna kimbunga.^b

Hakuna bua linalozaa nafaka iliyokomaa;^c

Bua lolote linalochipuka halitokezi unga.

Unga wowote wanaopata, utamezwa na wageni.^d

8 Waisraeli watamezwa.^e

Sasa watakuwa miongoni mwa mataifa,^f

Kama chombo ambacho hakitakikani.

9 Kwa maana wamepanda kwenda Ashuru,^g kama punda mwitu aliye peke yake.

Waefraimu wamekodi wopenzi.^h

10 Ingawa wanawakodi kutoka miongoni mwa mataifa,

Sasa mimi nitawazingira; Wataanza kutesekaⁱ kwa sababu ya mzigo walio

twikwa na mfalme na wakuu.

11 Kwa maana Waefraimu wamezidisha madhabahu ili watende dhambi.^j

Zikawa madhabahu walizotumia kutenda dhambi.^k

SURA YA 8

a Kum 32:21, 22

2Fa 17:18

b Met 22:8

c Isa 17:11

d Kum 28:15, 33

e 2Fa 15:29

2Fa 18:11

Yer 50:17

f Law 26:33

g 2Fa 15:19

Eze 23:4, 5

Ho 5:13

Ho 12:1

h Eze 23:9

i 2Fa 14:26

1Nya 5:26

j Isa 10:10, 11

k Ho 12:11

Safu ya 2

a 2Fa 17:15

Ne 9:26

b Isa 1:11

Amo 5:22

c Ho 9:9

Amo 8:7

d Ho 7:16

Ho 9:3

e Kum 32:18

f 1Fa 12:25, 31

g 2Nya 26:9, 10

h 2Fa 18:13

2Nya 36:17, 19

Yer 17:27

Yer 34:7

SURA YA 9

i Ho 10:5

j Eze 23:4, 5

Ho 4:12

k Ho 2:12

Mik 1:7

l Ho 2:8, 9

Amo 5:11

m Law 20:22

Kum 28:63, 64

Yos 23:15, 16

1Fa 9:6, 7

n 2Fa 17:6

o Hes 15:5

Hes 28:14

Yoe 1:13

12 Niliwaandikia mambo mengi ya sheria* yangu, Lakini waliyaona kuwa mambo ya ajabu.^a

13 Wananitolea zawadi za dhahihu, nao wanakula nyama,

Lakini mimi Yehova sipe ndezwi nazo.^b

Sasa nitakumbuka kosa lao na kuwaadhibu kwa sababu ya dhambi zao.^c

Wamegeuka na kurudi* Misri.^d

14 Waisraeli wamemsahau Muumba wao^e na kuje ngema mahekalu,^f

Na watu wa Yuda wamezidisha majiji yenye ngome.^g

Lakini nitashusha moto kwenye majiji yao,

Nao utateketeza minara iliyo katika kila jiji.^h

9 "Msishangilie, enyi Waisraeli,ⁱ

Msishangilie kama mataifa.

Kwa maana kwa ukahaba* wenu mmetangatanga na kumwacha Mungu wenu.^j

Mmependa malipo ya kahaba katika kila kiwanja cha kupuria nafaka.^k

2 Lakini uwanja wa kupuria na shinkizo la divai havitawalisha,

Na divai mpya itawaishia.^l

3 Hawataendelea kukaa katika nchi ya Yehova;^m

Badala yake, Waefraimu watarudi Misri,

Nao watakuwa vitu visivyo safi kule Ashuru.ⁿ

4 Hawatammiminia tena Yehova matoleo ya divai;^o

8:12 *Au "mafundisho." **8:13** *Au labda, "Watarudi." **9:1** *Au "umalaya."

8:5 *Au "kushindwa kuwa safi?"

Dhabihu zao hazitampe-
ndeza.^a

Dhabihu hizo ni kama
mkate wa maombolezo;
Wote wanaoula watajicha-
fua.

Kwa maana mkate wao ni
wao peke yao;*

Hautaletwa katika nyumba
ya Yehova.

5 Mtafanya nini katika siku
ya mkutano, *

Katika siku ya sherehe ya
Yehova?

6 Kwa maana tazama! wa-
talazimika kukimbia kwa
sababu ya maangamizi.^b
Misri itawakusanya pamo-
ja,^c na Memfisi itawa-
zika.^d

Upupu utamiliki vitu
vyao vya fedha vyenye
thamani,

Na vichaka vya miiba vi-
takua katika mahema
yao.

7 Siku za kuwajibika zita-
kuja,^e

Siku za kulipiza kisasi
zita kuja,

Na Waisraeli watajua
jambo hilo.

Nabii wao atakuwa mjinga,
na mtu anayeongozwa
na roho atashikwa na
wazimu;

Kwa sababu makosa yenu
ni mengi, uhasama dhidi
yenu ni mkubwa.”

8 Mlinzi^f wa Efraimu aliku-
wa na Mungu wangu.^g

Lakini sasa njia zote za
manabii wake^h ni kama
mitego ya mwindaji wa
ndege;

SURA YA 9

a Isa 1:11

b Ho 7:13

c Ho 7:16
Ho 8:13

d Yer 2:14, 16

e Isa 10:3

f Isa 21:6, 8
Yer 6:17
Eze 33:7

g 1Fa 17:1
2Fa 2:14

h 1Fa 18:19

Safu ya 2

a Amu 19:22
Amu 20:4-6
Ho 10:9

b Ho 8:13

c Yer 2:2

d Hes 25:1-3
Kum 4:3
Zb 106:28

e 1Fa 16:31
Yer 11:13

f Kum 28:15, 18

g Kum 28:32
Kum 32:25

h Kum 31:17
2Fa 17:18

i Eze 28:12

j Ho 4:15
Ho 12:11
Amo 5:5

Kuna uhasama katika nyu-
mba ya Mungu wake.

9 Wamezama ndani sana ka-
tika maangamizi, kama
ilivyokuwa kule Gibeaa.^a

Atakumbuka kosa lao na
kuwaadhibu kwa sababu
ya dhambi zao.^b

10 “Niliwapata Waisraeli
kama zabibu nyikani.^c

Kama matunda ya kwanza
ya tini niliwaona mababu
zenu.

Lakini walienda kwa Baali
wa Peori;^d

Walijiweka wakfu kwa kile
kitu cha aibu,^{*e}

Wakawa chukizo kama
kitu walichokipenda.

11 Utukufu wa Waefraimu
unaruka mbali kama
ndege;

Hakuna kuzaa, hakuna mi-
mba, na hakuna kushika
mimba.^f

12 Hata wakiwalea watoto,
Nitawaangamiza asibaki
mtu yeyote;^g

Naam, ole wao nitakapo-
waacha!^h

13 Waefraimu, waliopandwa
malishoni, walikuwa
kama Tiro kwangu;ⁱ

Sasa lazima Waefraimu
wawalete wana wao ili
wachinjwe.”

14 Ee Yehova, wape unacho-
paswa kuwapa;

Tumbo la uzazi linalohari-
bu mimba na matiti yali-
yokauka.*

15 “Walifanya uovu wao
wote kule Gilgali,^j kwa
maana nilianza kuwa-
chukia huko.

9:4 *Au “ni wa nafsi yao wenyewe.”

9:5 *Au “karamu yenu iliyoa mriwa.”

9:10 *Au “mungu wa aibu.” 9:14 *Au
“yalionyauka.”

Nitawafukuza katika nyumba yangu kwa sababu ya matendo yao maovu.^a Sitawapenda tena;^b Wakuu wao wote ni wakaidi.

16 Waefraimu wataangushwa chini.^c

Mzizi wao utakauka, nao hawatazaa tunda lolote. Hata wakizaa, nitawaua wazao wao wanaowape-nda.”

17 Mungu wangu atawakataa, Kwa maana hawajamsikiliza,^d

Nao watakuwa wakimbizi miongoni mwa mataifa.^e

10 “Waisraeli ni mzabibu ulioharibika* unaozaa matunda.^f

Kadiri matunda yao yanavyoongezeka, ndivyo wanavyozidisha madhabahu zao;^g

Kadiri nchi yao inavyozaa vizuri, ndivyo fahari ya nguzo zao takatifu inavyozidi kuongezeka.^h

2 Moyo wao una ufiki;* Sasa watapatikana na hatia.

Kuna yule atakayebomoa madhabahu zao na kuharibu nguzo zao.

3 Watasema, ‘Hatuna mfalme,ⁱ kwa sababu hatujamwogopa Yehova. Na mfalme atatufanyia nini?’

4 Wanasema maneno matupu, wanatoa viapo vya uwongo,^j na kufanya maagano;

Basi maamuzi wanayofanya ni kama magugu ye-

10:1 *Au labda, “unaoenea.” 10:2 *Au “hila; udanganyifu.”

SURA YA 9

a Law 26:27, 33
2Fa 17:18
Amo 5:27

b Kum 29:19, 20

c Isa 7:8

d 2Fa 17:14, 15
Zek 1:4

e Kum 28:64
Amo 9:9

SURA YA 10

f Isa 5:3, 4

g Ho 8:11
Ho 12:11

h Ho 8:4

i Ho 3:4
Ho 13:11

j 2Fa 17:4

Safu ya 2

a Amo 5:7
Amo 6:12

b 1Fa 12:28, 29
Ho 4:15
Ho 8:5
Amo 3:14

c 2Fa 17:3
Ho 5:13

d Mik 6:16

e 2Fa 17:4

f Ho 4:15

g 1Fa 12:28-30
Mik 1:5

h Amo 7:9

i 2Fa 23:15

j Lu 23:30
Ufu 6:16

k Amu 20:4-6
Ho 9:9

nye sumu kwenye mitaro iliyo shambani.^a

5 Wakaaji wa Samaria wataogopa kwa sababu ya sanamu ya ndama ya Beth-aveni.^b

Watu wake wataiombe-
lezea,

Na pia makuhani wa mungu huyo wa kigeni waliokuwa wakiishangilia pamoja na utukufu wake,

Kwa maana itachukuliwa na kupelekwa uhamishoni.

6 Itapelekwa Ashuru kama zawadi kwa mfalme mkuu.^c

Waefraimu wataaibishwa, Na Waisraeli wataaibika kwa sababu ya ushauri waliofuata.^d

7 Watu wa Samaria na mfalme wao hakika wataa-
ngamizwa,^e

Kama kijiti kilichokwanyuliwa kinachoelea juu ya maji.

8 Mahali pa juu pa Beth-aveni,^f dhambi ya Waisraeli,^g pataharibiwa kabisa.^h

Miiba na michongoma itamea juu ya madhabahu zao.ⁱ

Watu wataambia milima, ‘Tufuniken!’

Na vilima, ‘Tuangukieni!’^j

9 Enyi Waisraeli, mmetenda dhambi tangu kule Gibebea.^k

Nao wanaendelea kutenda dhambi huko.

Vita havikuwaangamiza kabisa wana wa ukosefu wa uadilifu kule Gibebea.

10:7 *Tnn., “watanyamazishwa.”

10 Pia nitawatia nidhamu wakati ninaopenda.

Na mataifa yatakusanyika dhidi yao,

Makosa yao mawili yatakapofungiliwa juu yao.*

11 Waefraimu walikuwa kama ndama jike aliyezoezwa aliyependa kupura,

Basi niliihurumia shingo yake nzuri.

Sasa nitamfanya mtu fulani apande juu ya Waefraimu na kuwaendesha.*^a

Watu wa Yuda watalima; watu wa Yakobo watalimilia.

12 Jipandieni mbegu kwa uadilifu na mvune upendo mshikamanifu.

Jilimieni shamba linalofaa kwa kilimo^b

Maadamu wakati upo wa kumtafuta Yehova,^c

Mpaka atakapokuja na kuwafundisha uadilifu.^d

13 Lakini mmelima uovu, Mmevuna ukosefu wa uadilifu,^e

Nanyi mmekula matunda ya udanganyifu;

Kwa sababu mmetumaini njia yenu wenyewe,

Mmewatumaini mashujaa wenu wengi.

14 Fujo itatokea dhidi ya watu wenu,

Na majiji yenu yenye ngo-me yataharibiwa yote,^f

Kama Shalmani alivyoharibu kabisa nyumba ya Arbeli,

Katika siku ya vita, akina mama walipondwapo-

SURA YA 10

a 2Fa 17:6

b Yer 4:3, 4

c Isa 55:6
Amo 5:4d Kum 32:2
Isa 45:8e Met 22:8
Ho 8:7
Gal 6:7

f 2Fa 18:9, 10

Safu ya 2

a Amo 7:9

b 2Fa 18:9, 10

SURA YA 11

c Kum 7:8

d Kut 4:22
Mt 2:14, 15

e Isa 30:9-11

f Amu 2:13
Amu 3:7
1Fa 16:30-32
1Fa 18:19
2Fa 17:13, 16
Ho 2:13g 1Fa 12:32, 33
Ho 13:1, 2

h Kum 8:2

i Kum 1:31
Kum 33:27
Isa 46:3

j Isa 63:9

k 2Fa 17:3

l 2Fa 17:13, 14
Amo 4:6

m Lam 26:31

ndwa pamoja na watoto wao.

15 Hivyo ndivyo mtakavyotendewa, enyi wakaaji wa Betheli,^a kwa sababu ya uovu wenu uliozidi.

Kwa hakika mfalme wa Israeli ataangamizwa* wakati wa mapambazuko.^b

11 "Israeli alipokuwa mvulana, nilimpenda,^c

Nikamwita mwanangu atoke Misri.^d

2 Kadiri walivyowaita,* Ndivyo walivyoenda mbali nao.^e

Waliendelea kutoa dhahihu kwa sanamu za Baali^f Na kutoa dhahihu kwa sanamu za kuchongwa.^g

3 Lakini mimi ndiye niliyewafundisha Waefraimu kutembea,^h nikawabeba mikononi mwangu;ⁱ

Lakini hawakutambua kwamba niliwaponya.

4 Niliendelea kuwawata kwa kamba za wanadamu,* kwa kamba za upendo;^j

Nami nilikuwa kwao kama mtu anayeinua nira kutoa kwenye mataya yao, Na kwa upole nikamletea kila mmoja wao chakula.

5 Hawatarudi katika nchi ya Misri, lakini watatawaliwa na Ashuru,^k

Kwa sababu walikataa kunirudia.^l

6 Na upanga utavuma dhidi ya majiji yao^m

10:15 *Tnn., "atanyamazishwa." **11:2**

*Yaani, manabii na watu wengine waliotumwa kuwafundisha Waisraeli. **11:4** *Au "kamba za fadhili," kama zile zina-zotumiwa na mzazi.

10:10 *Yaani, watakapobeba adhabu yao kama nira. **10:11** *Au "kuwafunga nira."

Na kuharibu makomeo yao na kuwanyafua kwa sababu ya njama zao.^a

7 Watu wangu wana mwelekeo wa kutokuwa waaminifu kwangu.^b

Ingawa waliwaita wapande juu, * hakuna yeyote anayeynuka.

8 Enyi Waefraimu, kwa nini niwaache?^c

Enyi Waisraeli, kwa nini niwatie mikononi mwa maadui wenu?

Kwa nini niwatendee kama Adma?

Kwa nini niwafanye kama Seboiimu?^d

Moyo wangu umebadilika; Na pia nimechochewa kuwahurumia.^e

9 Sitamwaga hasira yangu inayowaka.

Sitawaangamiza tena Waefraimu,^f

Kwa maana mimi ni Mungu, mimi si mwanadamu,

Mtakatifu aliye miongoni mweni;

Nami sitawashambulia kwa hasira.

10 Watatembea wakimfuata Yehova, naye atanguruma kama simba;^g

Atakaponguruma, wanawe watakuja wakitetemeka kutoka magharibi.^h

11 Watatoka Misri wakitetemeka kama ndege,

Kama njiwa kutoka nchi ya Ashuru;ⁱ

Nami nitawapa makao katika nyumba zao,^{**} asema Yehova.^j

11:7 *Yaani, kwenye ibada iliyokwezwa.
11:11 *Tnn., "nitafanya wakae katika nyumba zao."

SURA YA 11

a Isa 31:1

b Zb 78:57, 58
Yer 3:6

c Ho 6:4

d Mwa 10:19
Kum 29:22, 23

e Kum 32:36
Yer 31:20

f Yer 30:11

g Yoe 3:16

h Zek 8:7

i Isa 11:11, 12
Isa 60:8, 9
Zek 10:10

j Yer 23:6
Eze 28:25, 26
Eze 37:21
Amo 9:14

Safu ya 2

a Mik 6:12

b 2Fa 18:1, 6
2Nya 29:1, 2
Ho 4:15

SURA YA 12

c 2Fa 15:19
Ho 8:9

d 2Fa 17:4

e 2Fa 17:19
Yer 2:35
Ho 4:1
Mik 6:2

f Isa 3:11

g Mwa 25:26

h Mwa 32:28

i Mwa 32:24-26

j Mwa 28:13, 19

k Mwa 28:16
Mwa 32:30

l Kut 3:15

m Isa 31:6
Ho 14:1
Yoe 2:12, 13

n Kum 16:20
Mik 6:8

12 "Waefraimu wamenizingira wakisema uwongo, Na nyumba ya Israeli kwa udanganyifu.^a

Lakini watu wa Yuda bado wanazunguka huku na huku* pamoja na Mungu, Nao ni waaminifu kwangu mimi, niliye Mtakatifu Zaidi."^b

12 "Waefraimu wanakula upepo.

Wanaukimbiza upepo wa mashariki siku nzima.

Wanazidisha uwongo na ukatili.

Wanafanya agano na Ashuru^c na kupeleka mafuta Misri.^d

2 Yehova ana kesi dhidi ya watu wa Yuda;^e

Atawafanya wazao wa Yakobo wawajibike kulingana na njia zao, Naye atawalipa kulingana na matendo yao.^f

3 Wakiwa tumboni, Yakobo alimshika kisigino ndugu yake,^g

Na kwa nguvu zake alishindana na Mungu.^h

4 Aliendelea kushindana na malaika na kumshinda.

Alilia na kumsihi apate kibali chake."ⁱ

Alimkuta Yakobo kule Betheli, na huko akazungumza nasi,^j

5 Yehova Mungu wa majeshi,^k

Yehova ndilo jina lake la ukumbusho.*^l

6 "Basi mrudieni Mungu wenu,^m

Dumisheni upendo mshikamanifu na haki,ⁿ

11:12 *Au "wanatembea." 12:5 *Au "anakumbukwa kwa jina hilo."

Na sikuzote mumtumaini
Mungu wenu.

7 Lakini mfyanyiashara
ana mizani ya udanga-
nyifu mkononi mwake;
Anapenda kuwapunja
watu.^a

8 Waefraimu husema, 'Kwa
kweli, tumetajirika;^b
Tumepata utajiri.^c

Na katika kazi zetu zote za
jasho, hawatapata kosa
au dhambi yoyote.'

9 Lakini mimi ni Yehova Mu-
ngu wenu kuanzia* mli-
pokuwa nchini Misri.^d

Nitawafanya mkae tena ka-
tika mahema
Kama ilivyokuwa katika
siku za kipindi kilichoa-
mriwa.[#]

10 Niliongea na manabii,^e
Nikazidisha maono yao,
Nami nikasimulia mifano
kupitia manabii.

11 Kule Gileadi watu wame-
tenda kwa udanganyifu*^f
na uwongo.

Huko Gilgali wametoa dha-
bihu za ng'ombe dume,^g
Na madhabahu zao ni
kama marundo ya mawe
katika mitaro iliyo sha-
mbani.^h

12 Yakobo alikimbilia eneo*
la Aramu;^{#i}

Israeli/ alitumikia huko ili
apate mke,^k
Na ili apate mke, alichu-
nga kondoo.^l

13 Na kupitia nabii, Yehova
aliwapandisha Waisraeli
kutoka Misri,^m

12:9; 13:4 * Au "tangu." 12:9 # Au lab-
da, "sherehe." 12:11 * Au "wametenda
uchawi; mazingaombwe." 12:12 * Tnn.,
"shamba." # Au "Siria."

SURA YA 12

a Amo 8:5, 6
Mik 2:1, 2

b Ufu 3:17

c Kum 8:17-19

d Kut 20:2
Ho 13:4

e 1Fa 17:1
2Fa 17:13
Amo 7:14, 15

f Ho 6:8

g Ho 9:15
Amo 4:4

h 2Fa 17:9, 10
Ho 8:11
Ho 10:1

i Mwa 28:5
Kum 26:5

j Mwa 32:28

k Mwa 29:18

l Mwa 31:38

m Kut 12:50, 51
Zb 77:20

Safu ya 2

a Yos 24:17
1Sa 12:8

b 2Fa 17:9-11
Eze 23:4, 5

c Kum 28:37

SURA YA 13

d Yos 17:17

e 2Fa 17:16
Ho 11:2

f Ho 2:8

g 1Fa 12:26, 28
1Fa 19:18

h Kut 20:2
Ho 12:9

Na kupitia nabii, walili-
ndwa.^a

14 Waefraimu wamemchuki-
za sana Mungu;^b

Wataendelea kuwa na ha-
tia ya damu;

Bwana wao atawaadhibu
kwa sababu ya kumwai-
bisha."^c

13 "Waefraimu walipoo-
ngea, watu walitete-
meka;

Walikuwa maarufu mio-
ngoni mwa Waisraeli.^d

Lakini wakawa na hatia
kuhusiana na Baali,^e nao
wakafa.

2 Sasa wanazidisha dhambi
yao

Na kutengeneza sanamu
za madini* kwa fedha
yao;^f

Wanatengeneza sanamu
kwa ustadi, hizo zote ni
kazi za mafundi.

Wanasema hivi mbele ya
sanamu hizo: 'Watu wa-
naotoa dhabihu na wa-
busu ndama hawa.'^g

3 Kwa hiyo watakuwa kama
ukungu wa asubuhi,

Kama umande unaotowe-
ka mapema,

Kama makapi yanayopepe-
rushwa na dhoruba ku-
toka kwenye uwanja wa
kupuria,

Na kama moshi unaotoka
katika bomba la moshi
paani.

4 Lakini mimi ni Yehova Mu-
ngu wenu kuanzia* mli-
pokuwa nchini Misri;^h

Hamkunjua Mungu mwi-
ngine yeyote isipokuwa
mimi,

13:2 * Tnn., "za kuyeyushwa."

Na hakuna mwokozi mwingine yeyote ila mimi.^a

- 5** Niliwajua mlipokuwa nyikani,^b katika nchi yenye ukame.
- 6** Walitosheka na malisho yao,^c
Walitosheka moyo wao ukawa na kiburi.
Na kwa hiyo wakanisau.^d
- 7** Nitakuwa kama mwanasimba kwao,^e
Kama chui anayevizianjiani.
- 8** Nitawarukia kama dubu aliyepoteza watoto wake, Nami nitavirarua vifua vyao.*
Na huko nitawanyafua kama simba;
Mnyama wa mwituni atawararua vipandevipande.
- 9** Atawaangamiza, enyi Waisraeli,
Kwa sababu mmenigeuka, mmemgeuka msaidizi wenu.
- 10** Yuko wapi sasa mfalme wenu ili awaokoe katika majiji yenu yote,^f
Na watawala* wenu ambao mlisema kuwahusu, "Tupe mfalme na wakuu"?^g
- 11** Kwa hasira nikawapa mfalme,^h
Nami nitamwondoa kwa ghadhabu.ⁱ
- 12** Kosa la Waefracimu limefungwa kabisa;*
Dhambi yao imewekwa akiba.
- 13** Watashikwa na uchungu wa kuzaa.

13:8 *Tnn., "chumba cha moyo wao."
13:10 *Tnn., "waamuzi." 13:12 *Au "li-mehifadhiwa."

SURA YA 13

a Isa 43:11
Isa 45:21, 22

b Kum 2:7
Kum 32:9, 10

c Ne 9:25

d Kum 6:10-12
Kum 8:12-14
Kum 32:15, 18
Isa 17:10

e Ho 5:14

f 1Sa 8:19, 20

g 1Sa 8:4, 5

h 1Sa 8:7
1Sa 12:13

i 1Sa 12:25
2Fa 17:4
Yer 52:11

Safu ya 2

a Isa 25:8
Isa 26:19

b 1Ko 15:55

c Ufu 20:13, 14

d 2Fa 17:20

e 2Fa 17:18
Amo 3:9, 10

f Eze 20:21

g Isa 7:8

SURA YA 14

h 2Nya 30:6
Isa 55:6, 7
Ho 12:6
Yoe 2:12, 13

i Mik 7:18

Lakini wao ni mtoto asiye na hekima;
Hatoki tumboni wakati wa kuzaliwa ufikapo.

- 14** Nitawakomboa kutoka katika angu za Kaburi;*
Nitawaokoa kutoka katika kifo.^a

Ewe Kifo, yako wapi mawimivu yako makali?^{#b}

Ewe Kaburi, yako wapi maangamizi yako?^c

Macho yangu yatazuiwa yasione huruma.

- 15** Hata wakisitawi kati ya matete,

Upepo wa mashariki utakuja, upepo wa Yehova, Utakuja kutoka jangwani, kukausha kisima chao na chemchemi yao.

Huyo atapora hazina ya vitu vyao vyote vyenye thamani.^d

- 16** Watu wa Samaria watahesabiwa kuwa na hatia,^e kwa sababu wamemwasi Mungu wao.^f

Watauawa kwa upanga,^g

Watoto wao watapondwapondwa,

Na wanawake wao wenye mimba watapasuliwa tumbo."

- 14** "Enyi Waisraeli, mrudieni Yehova Mungu wenu,^h

Kwa maana mmejikwaa kwa sababu ya kosa lenu.

- 2** Mrudieni Yehova kwa maneno haya,
Mwambieni, 'Tusamehe kosa letu' na ukubali ya-liyo mema,

13:14 *Au "Sheoli." Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "iko wapi michomo yako?"

Nasi tutatoa sifa ya mi-domo yetu^a kama vile ambavyo tungetoa ng'ombe dume wachanga.*

- 3** Ashuru haitatuokoa.^b
Hatutapanda farasi,^c
Na hatutaziambia tena kazi za mikono yetu,
“Ee Mungu wetu!”
Kwa sababu ni wewe unayemwonyesha yatima re-hema.”^d
- 4** Nitauponya ukosefu wao wa uaminifu.^e
Nitawapenda kwa hiari yangu mwenyewe,^f
Kwa sababu hasira yangu imegeuka na kuwaacha.^g
- 5** Nitakuwa kama umande kwa Waisraeli;
Watachanua kama yungiyungi
Nao wataipenyeza chini mizizi yao kama miti ya Lebanoni.
- 6** Vitawi vyao vitasambaa,
Fahari yao itakuwa kama ya mzeituni,

14:2 *Tnn., “nasi tutakutolea ng'ombe dume wachanga wa midomo yetu.”

SURA YA 14

a Ebr 13:15

b Ho 5:13

c Isa 31:1

d Kum 10:17, 18

e Zb 103:3
Isa 57:18

f Sef 3:17

g Isa 12:1

Safu ya 2

a Zek 8:12

b Ho 14:3

c Yer 31:18

d Kum 32:4

HOSEA 14:3 – YOELI Yaliyomo

Na manukato yao kama ya Lebanoni.

- 7** Watakaa tena chini ya kivuli chake.
Watapanda nafaka na kutokeza matumba kama mzabibu.^a
Umaarufu* wao utakuwa kama wa divai ya Lebanoni.
- 8** Waefraimu watasema,
“Tunahitaji tena sanamu za nini?”^b
Nitawajibu na kuwalinda.^c
Nitakuwa kama mberoshi unaositawi.
Mtapata matunda yenu kutoka kwangu.”
- 9** Ni nani aliye na hekima?
Na aelewe mambo haya.
Ni nani aliye na busara? Na ayajue mambo hayo.
Kwa maana njia za Yehova zimenyooka,^d
Na waadilifu watatembea katika njia hizo;
Lakini watenda dhambi watajikwaa humo.

14:7 *Tnn., “Ukumbusho.”

YOELI

YALIYOMO

- 1 Shambulizi kali la wadudu (1-14)
“Siku ya Yehova iko karibu” (15-20)
Nabii amlilia Yehova (19, 20)
- 2 Siku ya Yehova na jeshi lake kubwa (1-11)
Wasihiwa wamrudie Yehova (12-17)
“Irarueni mioyo yenu” (13)
Yehova awajibu watu wake (18-32)
“Nitaimimina roho yangu” (28)
Maajabu mbinguni na duniani (30)

Wale wanaoliitia jina la Yehova wataokolewa (32)

- 3 Yehova ahukumu mataifa yote (1-17)
Bonde la Yehoshafati (2, 12)
Bonde la uamuzi (14)
Yehova, ngome kwa Israeli (16)
Yehova awabariki watu wake (18-21)

1 Neno la Yehova lililomjia Yoeli* mwana wa Pethueli:

2 “Sikilizeni jambo hili, enyi wazee,

Sikilizeni kwa makini, enyi wakaaji wote wa nchi.*

Je, jambo kama hili lime-wahi kutokea katika siku zenu

Au katika siku za mababu zenu?^a

3 Wasimulieni wana wenu jambo hilo,

Na acheni wana wenu wa-wasimulie wana wao ku-lihusu,

Na wana wao wasimulie ki-zazi kitakachofuata.

4 Kilichoachwa na nzige wa-naokula sana, kimeliwa na nzige wanaoruka kati-ka makundi;^b

Na kilichoachwa na nzige wanaoruka katika maku-ndi, kimeliwa na tunutu;

Na kilichoachwa na tunu-tu, kimeliwa na parare* wanaokula sana.^c

5 Enyi walevi,^d amkeni mlie!

Pigeni mayowe, ninyi nyo-te mnaokunywa divai, Kwa sababu divai tamu imeondolewa vinywani mwenu.^e

6 Kwa maana taifa limeiva-mia nchi yangu, lenye nguvu na lisilo na idadi.^f

Meno yake ni meno ya si-мба,^g na mataya yake ni ya simba.

7 Limeharibu mzabibu wa-ngu na kuacha mtini wa-ngu ukiwa kisiki,

Limebambua magamba yote na kuyatupa pe-mbeni,

SURA YA 1

a Yoe 2:2

b Kut 10:14, 15

c Yoe 2:25

d Isa 28:1
Amo 6:6

e Kum 28:39

f Yoe 2:2

g Ufu 9:7, 8

Safu ya 2

a Law 2:1

b Kut 29:40

c Law 26:20

d Kum 28:39, 40

e Law 26:20

f Kut 30:19, 20

Na kuacha matawi yake ya-kiwa meupe.

8 Ombolezeni kwa sauti kama bikira* aliyevaa nguo za magunia

Anayeomboleza kwa ajili ya bwana harusi[#] wa uja-na wake.

9 Toleo la nafaka^a na toleo la kinywaji^b hayapo tena kwenye nyumba ya Yehova;

Makuhani, wahudumu wa Yehova, wanaomboleza.

10 Mashamba yameharibiwa, ardhi inaomboleza;^c

Kwa kuwa nafaka imeha-ribiwa, divai mpya ime-kauka, mafuta yameto-weka.^d

11 Wakulima wamefadhaika, watunzaji wa mizabibu wanapiga mayowe,

Kwa sababu ya ngano na shayiri;

Kwa maana mavuno ya shambani yameharibika.

12 Mzabibu umekauka, Mtini umenyauka.

Mkomamanga, mtende, na mtofaa,

Miti yote shambani ime-kauka;^e

Kwa maana badala ya kuwa na shangwe, watu wameshikwa na aibu.

13 Vaeni* nguo za magunia na kuomboleza,[#] enyi makuhani;

Pigeni mayowe, enyi wahu-dumu wa madhabahu.^f

Ingeni na kulala hekaluni usiku kucha mkiwa mmevaa nguo za magu-

1:1 *Maana yake “Yehova Ni Mungu.”

1:2 *Au “dunia.” 1:4 *Au “panzi.”

1:8 *Au “mwanamwali.” #Au “mume.”
1:13 *Tnn., “Jifungeni.” #Tnn., “kujipi-ga vifua.”

nia, enyi wahudumu wa Mungu wangu;

Kwa maana matoleo ya nafaka^a na matoleo ya vinywaji^b hayaletwi tena katika nyumba ya Mungu wenu.

- 14** Tangazeni watu wafunge;* waiteni watu kwenye kusanyiko takatifu.^c

Wakusanyeni wazee, pamoja na wakaaji wote wa nchi,

Kwenye nyumba ya Yehova Mungu wenu,^d nanyi mlieni Yehova awasaidie.

- 15** Ole kwa sababu ya ile siku!

Kwa maana siku ya Yehova iko karibu,^e

Nayo itakuja kama maa-ngamizi kutoka kwa Mweza-Yote!

- 16** Je, chakula hakijaondolewa mbele ya macho yetu wenyewe,

Na shangwe na furaha kutoka katika nyumba ya Mungu wetu?

- 17** Mbegu* zimenyauka chini ya sepetu zao.

Maghala yamebaki ukiwa. Maghala ya nafaka yamebolewa, kwa maana nafaka imekauka.

- 18** Hata mifugo inalia kwa uchungu!

Makundi ya ng'ombe yanatangatanga huku na huku, kwa maana hayana malisho!

Na hata makundi ya kondoo yamepata adhabu.

- 19** Nitakuita wewe, Ee Yehova;^f

SURA YA 1

a Law 2:1

b Kut 29:40

c Yoe 2:15

d 2Nya 20:3,13

e Yoe 2:1
Sef 1:7,14
Sef 2:2
ZPe 3:10
Ufu 6:16,17

f Mik 7:7
Hab 3:18

Safu ya 2

SURA YA 2

a Eze 33:2,3
Amo 3:6

b Sef 1:14,16
Mal 4:1

c Amo 5:18,20

d Sef 1:15

e Yoe 1:6

f Yoe 1:19

g Mwa 2:8

Kwa maana moto umetekeleza kabisa malisho nyikani,

Na mwali wa moto ume-teketeza miti yote shambani.

- 20** Hata wanyama wa mwituni wanasubiri kwa hamu uwasaidie,
Kwa sababu vijito vya maji vimekauka

Na moto umeteketeza kabisa malisho nyikani.”

- 2** “Pigeni pembe Sayuni!^a
Pigeni kelele za vita katika mlima wangu mtakatifu.
Wakaaji wote wa nchi* na watetemeke,

Kwa maana siku ya Yehova inakuja!^b Iko karibu!

- 2** Ni siku ya giza na utusitusi,^c

Siku ya mawingu na utusitusi mzito,^d

Giza hilo litaenea kama nuru ya mapambazuko juu ya milima.

Kuna taifa lenye watu wengi na lenye nguvu;^e

Halijawahi kamwe kuwepo taifa kama hilo,

Na halitakuwepo tena kamwe taifa lingine kama hilo

Katika miaka yote ya viza-zi vyote.

- 3** Moto unateketeza kila kitu kilicho mbele yake,
Na vitu vilivyopo nyuma yake vinateketezwa na mwali wa moto.^f

Kabla halijapita nchi huwa kama bustani ya Edeni,^g

Lakini baada ya kupita nchi inabaki nyika iliyo ukiwa,

1:14 *Tnn., “Takaseni mfungo.” 1:17

*Au labda, “Tini zilizokaushwa.”

2:1 *Au “dunia.”

Na hakuna chochote kina-
choweza kuponyoka.

- 4** Linafanana na farasi,
Nao hukimbia kama farasi
wa vita.^a
- 5** Wanaporuka juu ya vilele
vya milima, sauti yao ni
kama ya magari ya vita,^b
Kama sauti ya moto mkali
unaoteketeza majani ma-
kavu.
Wao ni kama taifa lenye
nguvu lililojipanga ki-
vita.^c
- 6** Kwa sababu yao, mataifa
yatakuwa na maumivu
makali.
Kila uso utageuka na kuwa
mwekundu kwa sababu
yao.
- 7** Wanashambulia kama ma-
shujaa,
Wanapanda ukuta kama
wanajeshi,
Kila mmoja wao anae-
ndelea kufuata mwendo
wake mwenyewe,
Nao hawatoki katika njia
zao.
- 8** Hawasukumani;
Kila mtu hupiga mwendo
kwenye njia yake.
Baadhi yao wakiuawa kwa
silaha,
Wengine hawavunji safu
zao.
- 9** Wanaingia haraka jijini,
nao hukimbia ukutani.
Hupanda juu ya nyumba,
na kuingia kama mwizi
madirishani.
- 10** Nchi inatetemeka mbele
yao na mbingu kutiki-
sika.
Jua na mwezi vimekuwa
na giza,^d
Na nyota zimepoteza mwa-
ngaza wake.

SURA YA 2

a Ufu 9:7

b Ufu 9:9

c Met 30:27

d Yoe 2:31
Mt 24:29
Lu 21:25
Ufu 9:2

Safu ya 2

a Yoe 2:25

b Yoe 2:2

c Yer 30:7
Amo 5:18
Sef 1:15

d Ufu 6:16,17

e Yer 4:1
Ho 12:6
Ho 14:1, 2

f 1Sa 7:6
2Nya 20:3

g 2Fa 22:18,19
Zb 51:17
Isa 57:15

h 2Sa 1:11,12

i Isa 48:9

j Kut 34:6
Hes 14:18
Ne 9:17
Zb 106:44,45
Mik 7:18,19

k 2Nya 30:8,9
Yer 18:7,8
Sef 2:2,3

l Yoe 1:14

m Kut 19:10

11 Yehova atapaza sauti
mbele ya jeshi lake,^a kwa
maana jeshi lake ni ku-
bwa sana.^b

Kwa maana anayetokeleza
neni Lake ni mwenye
nguvu;

Kwa maana siku ya Yehova
ni kuu na inaogopesha
sana.^c

Ni nani anayeweza kuista-
himili?^d

12 "Hata sasa," asema Yeho-
va, "rudini kwangu kwa
moyo yenu yote,^e

Kwa kufunga^f na kulia na
kuomboleza.

13 Irarueni moyo yenu,^g
wala si mavazi yenu,^h

Nanyi mrudi kwa Yehova
Mungu wenu,

Kwa maana ni mwenye
huruma^{*} na rehema, si

mwepesi wa hasira,ⁱ
naye ana upendo mwingi
mshikamanifu,^j

Naye atafikiria upya^{*} msi-
ba aliokusudia kuleta.

14 Ni nani ajuaeye ikiwa ha-
tabadili nia na kuufikiria
upya^{*} k

Na kuwaachia baraka,

Ili mweze kumtolea

Yehova Mungu wenu
toleo la nafaka na toleo
la kinywaji?

15 Pigeni pembe Sayuni!

Tangazeni watu wafunge;^{*}
waiteni watu kwenye ku-
sanyiko takatifu.^l

16 Wakusanyeni watu; litaka-
seni kutaniko.^m

Wakusanyeni wanaume
wazee;^{*} wakusanyeni

2:13 *Au "neema." #Au "ataghairi ku-
husu." 2:14 *Au "kughairi." 2:15
*Tnn., "Takaseni mfunjo." 2:16 *Au
"wazee."

watoto wadogo na pia
watoto wanaonyonya.^a

Bwana harusi na atoke ka-
tika chumba chake cha
ndani, na bibi harusi ato-
ke katika chumba chake
cha bibi harusi.

17 Kati ya ukumbi na madha-
bahu^b

Acheni makuhani, wahu-
dumu wa Yehova, walie
na kusema:

'Ee Yehova, wahurumie
watu wako;

Usifanye urithi wako uwe
kitu cha kudharauliwa,
Kwa kuacha mataifa yawa-
tawale.

Kwa nini mataifa yaseme:
"Yuko wapi Mungu
wao?"^c

18 Kwa hiyo Yehova atakuwa
na bidii kwa ajili ya nchi
yake

Na kuwahurumia watu
wake.^d

19 Yehova atawajibu hivi
watu wake:

"Tazama, ninawaletea na-
faka na divai mpya na
mafuta,

Nanyi mtatosheka kabisa;^e
Sitafanya tena mshutumi-
we miongoni mwa ma-
taifa.^f

20 Nitamfukuza mbali nanyi
mkaaji wa kaskazini;

Nitamtawanya katika nchi
kavu iliyo ukiwa,
Walinzi wake wa mbele
kuelekea bahari ya ma-
shariki*^g

Na walinzi wake wa nyuma
kuelekea bahari ya ma-
gharibi.^h

SURA YA 2

a Kum 31:12
2Nya 20:3,13

b 2Nya 8:12

c Kum 32:26, 27
Zb 79:9,10
Mik 7:10

d Kum 32:36
Isa 60:10
Omb 3:22
Ho 11:8

e Isa 62:8,9
Amo 9:13
Mal 3:10

f Eze 34:29
Eze 36:15

Safu ya 2

a Isa 34:2,3

b Isa 30:23
Isa 51:3

c Eze 34:27

d Amo 9:14
Zek 8:12

e Isa 12:6
Zek 10:7

f Law 26:4
Kum 11:14

g Law 26:10
Amo 9:13
Mal 3:10

h Yoe 1:4

Na harufu yake mbaya ita-
panda juu,

Na uvundo wake utaende-
lea kupanda juu;^a

Kwa maana Atafanya
mambo makuu.'

21 Usiogope, Ee nchi.

Uwe na shangwe na fura-
ha, kwa maana Yehova
atafanya mambo makuu.

22 MsioCOPE, enyi wanyama
wa mwituni,

Kwa maana malisho ya nyi-
kani yatakuwa kijani ki-
bichi,^b

Na miti itazaa matunda;^c
Mitini na mizabibu itazaa
kwa wingi.^{*d}

23 Enyi wana wa Sayuni, iwe-
ni na shangwe na ku-
mshangilia Yehova Mu-
ngu wenu;^e

Kwa maana atawapa kiasi
kinachofaa cha mvua ya
vuli,

Naye atawaletea mvua
kubwa,

Mvua ya vuli na mvua ya
masika, kama ilivyokuwa
awali.^f

24 Viwanja vya kupuria vita-
jaa nafaka safi,

Na mashinikizo yatafu-
rika divai mpya na ma-
futa.^g

25 Nami nitafidia miaka
ambayo

Mazao yenu yaliliwa na
nzige wanaoruka katika
makundi, tunutu, parare
wanaokula sana, na nzi-
ge* wanaokula sana,
Jeshi langu kubwa ambalo
nililituma miongoni
mwenu.^h

2:20 *Yaani, Bahari ya Chumvi. #Yaani, Bahari ya Mediterania.

2:22 *Tnn., "kikamili." 2:25 *Au "panzi."

- 26** Kwa hakika mtakula na kutosheka,^a
Nanyi mtalisifu jina la Yehova Mungu wenu,^b
Ambaye ametenda mambo yenye kustaaabisha kwa niaba yenu;
Watu wangu hawataaibishwa tena kamwe.^c
- 27** Nanyi mtalazimika kujua kwamba nimo miongoni mwa Waisraeli^d
Na kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu^e—haku na mwingine!
Watu wangu hawataaibishwa tena kamwe.
- 28** Kisha nitaimimina roho yangu^f juu ya kila aina ya mwili,
Na wana wenu na mabinti wenu watatoa unabii,
Na wanaume wenu wazee wataota ndoto,
Na wanaume wenu vijana wataona maono.^g
- 29** Na hata juu ya watumwa wangu wa kiume na watumwa wa kike
Nitaimimina roho yangu siku hizo.
- 30** Nami nitafanya mambo ya ajabu* mbinguni na duniani,
Damu na moto na nguzo za moshi.^h
- 31** Jua litatiwa giza na mwezi utatiwa damu!ⁱ
Kabla ya kuja kwa ile siku ya Yehova iliyo kuu na yenye kuogopesha.^j
- 32** Na kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokolewa;^k

2:30 *Au "miujiza."

SURA YA 2

- a Law 26:5
b Kum 26:10, 11
c Sef 3:11
d Zb 46:5
e Law 26:11, 12
Eze 37:26, 27
f Isa 32:15
Isa 44:3
Eze 39:29
g Mdo 2:16-18
h Mdo 2:19, 20
i Mt 24:29
Mk 13:24, 25
Lu 21:25
Ufu 6:12
j Sef 1:14, 15
Mal 4:5
k Mdo 2:21
Ro 10:13

Safu ya 2

- a Oba 17

SURA YA 3

- b Kum 30:3
Yer 30:3
Eze 39:28
Amo 9:14
Sef 3:20
c Eze 38:22
Yoe 3:12
Sef 3:8
Zek 14:3
Ufu 16:14, 16
d Eze 35:10, 11
Sef 2:8, 9
e Oba 11
f Isa 23:12
Yer 47:4
Eze 25:15-17
Amo 1:9, 10
Zek 9:1, 2

Kwa maana kwenye Mlima Sayuni na katika Yerusalemu kutakuwa na wale wanaosalimika,^a kama Yehova alivyosema,
Waokokaji wanaoitwa na Yehova."

- 3** "Kwa maana tazama! kati-ka siku hizo na wakati huo,
Nitakapowarudisha mateka wa Yuda na Yerusalemu,^b
2 Nitakusanya pia mataifa yote
Na kuyaleta chini kwenye Bonde la* Yehoshafati.[#]
Na humo nitawahukumu^c
Kwa ajili ya watu wangu na urithi wangu Israeli,
Kwa maana waliwatawanya miongoni mwa mataifa,
Nao waligawana nchi yangu miongoni mwao.^d
3 Nao waligawana watu wangu kwa kura;^e
Walimuza mvulana ili wamlipe kahaba
Na kumuza msichana ili wanunue divai wanywe.
4 Pia, kwa nini mnanitendea hivi,
Enyi watu wa Tiro na Sidoni na maeneo yote ya Ufilisti?
Je, mnanilipiza kisasi kwa sababu ya jambo fulani?
Ikiwa mnanilipiza kisasi, Nitawalipiza kisasi haraka, naam, upesi.*^f

3:2 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."
#Maana yake "Yehova Ni Mwamuzi."
3:4 *Tnn., "Nitaleta kisasi haraka, upesi juu ya vichwa vyenu."

- 5** Kwa sababu mmechukua fedha na dhahabu yangu,^a
Nanyi mmepeleka hazina zangu bora kabisa kwenye mahekalu yenu;
- 6** Na watu wa Yuda na Yerusalemu mmewauza kwa Wagiriki,^b
Mkawaondoa na kuwapeleka mbali na eneo lao;
- 7** Tazameni, nitawachochea watoke mahali mlipowauza,^c
Nami nitawalipiza kisasi.*
- 8** Nitawauza wana wenu na mabinti wenu kwa watu wa Yuda,^d
Nao watawauza kwa wanaume wa Sheba, kwa taifa lililo mbali sana;
Kwa maana Yehova mwenyewe amesema hilo.
- 9** Tangazeni hili miongoni mwa mataifa:^e
'Jitayarisheni kwa ajili ya* vita! Wachocheeni wanaume hodari!
Wanajeshi wote na wakari-bie, acheni wapige mwendof
- 10** Yafueni majembe yenu yawe mapanga na miundu yenu iwe mikuki.
Aliye dhaifu na aseme:
"Nina nguvu."
- 11** Njoooni msaidie, enyi mataifa yote jirani, kusanyikeni pamoja!"^g
Ee Yehova, wateremshe mahali hapo wenyewe nguvu* wako.

3:7 *Tnn., "Nitaleta kisasi juu ya vichwa vyenu." 3:9 *Tnn., "Takaseni." 3:11 *Au "mashujaa."

SURA YA 3

a 2Nya 21:16, 17

b Kum 28:32
Eze 27:8, 13c Isa 11:11, 12
Isa 43:5, 6
Isa 49:12
Yer 23:7, 8
Eze 34:12

d Oba 19, 20

e Isa 34:1, 2

f Eze 38:7

g Eze 38:9
Sef 3:8
Ufu 16:14

Safu ya 2

a Zb 76:8, 9
Yoe 3:2b Isa 63:3
Ufu 14:18-20c Isa 34:2
Sef 1:14

d Zb 50:15

e Zek 8:3

f Isa 4:3

g Isa 60:18
Nah 1:15
Zek 14:21h Amo 9:13
Zek 9:17

- 12** "Mataifa na yachochee na kuja kwenye Bonde la* Yehoshafati;
Kwa maana nitaketi huko ili kuyahukumu mataifa yote jirani.^a
- 13** Tieni mundu, kwa maana mavuno yamekomaa.
Teremkeni na kuyakanyaga, kwa maana shinikizo la divai limejaa.^b
Mitungi inafurika, kwa sababu uovu wao ni mwingi.
- 14** Umati, umati umo katika bonde la* uamuzi,
Kwa maana siku ya Yehova iko karibu katika bonde la* uamuzi.^c
- 15** Jua na mwezi vitakuwa giza,
Na nyota zitapoteza mwan-gaza wake.
- 16** Na Yehova atanguruma kutoka Sayuni,
Atapaza sauti yake kutoka Yerusalemu.
Na mbingu na dunia zitatikisika;
Lakini Yehova atakuwa kimbilio kwa watu wake,^d
Ngome kwa watu wa Israeli.
- 17** Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu, ninayekaa Sayuni, mlima wangu mtakatifu.^e
Yerusalemu litakuwa mahali patakatifu,^f
Na wageni hawatapita tena humo.^g
- 18** Siku hiyo milima itadondosha divai tamu,^h
Vilima vitatiririka maziwa,

3:12 *Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

3:14 *Au "nchi tambarare ya chini ya."

Na vijito vyote vya Yuda
vitatiririka maji.

Kutoka katika nyumba ya
Yehova kijito kitatiri-
rika,^a

Nacho kitanywesha Bonde
la * Miti ya Mishita.

19 Lakini Misri itakuwa
ukiwa,^b

Na Edomu itakuwa nyika
iliyo ukiwa,^c

Kwa sababu ya ukatili

3:18 * Au "Nchi Tambarare ya Chini ya."

SURA YA 3

a Eze 47:1

Ufu 22:1

b Isa 19:1

c Yer 49:17

Safu ya 2

a Eze 25:12, 13

b Amo 1:11

Oba 10

c Zb 48:8

Isa 33:20

Isa 60:15

Amo 9:15

d Isa 4:4

Eze 36:25

Mik 7:18, 19

e Isa 24:23

Mik 4:7

waliowatenda watu wa
Yuda,^a

Katika nchi yao
walimwaga damu
isiyo na hatia.^b

20 Lakini Yuda itakaliwa
daima,

Na Yerusalemu kizazi baa-
da ya kizazi.^c

21 Damu yao niliyoiona kuwa
na hatia nitaiona kuwa

isiyo na hatia;^d
Na Yehova atakaa
Sayuni."^e

AMOSI

YALIYOMO

1 Amosi apokea ujumbe kutoka kwa
Yehova (1, 2)
Wahukumiwa kwa sababu ya kuasi
tena na tena (3-15)
Siria (3-5), Ufilisti (6-8), Tiro (9, 10),
Edomu (11, 12), Amoni (13-15)

2 Wahukumiwa kwa sababu ya
kuasi tena na tena (1-16)
Moabu (1-3), Yuda (4, 5),
Israeli (6-16)

3 Kutangaza hukumu ya Yehova (1-8)
Mungu afunua siri yake (7)
Ujumbe dhidi ya Samaria (9-15)

4 Ujumbe dhidi ya ng'ombe wa
Bashani (1-3)
Yehova adhihaki ibada ya uwongo
ya Waisraeli (4, 5)
Waisraeli wakataa nidhamu (6-13)
"Jitayarishe kukutana na Mungu
wako" (12)
'Mungu humwambia mwanadamu
mawazo Yake' (13)

5 Waisraeli ni kama bikira
aliyeanguka (1-3)

Mtafuteni Yehova, mwendelee
kuishi (4-17)

Chukieni maovu, pendeni
mema (15)

Siku ya Yehova itakuwa siku ya
giza (18-27)

Dhabihu za Waisraeli
zakataliwa (22)

6 Ole wao wasiojali! (1-14)
Vitanda vya pembe za tembo;
mabakuli ya divai (4, 6)

7 Maono yanayoonyesha mwisho
wa Israeli unakaribia (1-9)
Nzige (1-3), moto (4-6),
timazi (7-9)

Amosi aambiwa aache
kutabiri (10-17)

8 Maono ya kikapu kilichojaa matunda
ya wakati wa kiangazi (1-3)
Wakandamizaji washutumwiwa (4-14)
Njaa ya kiroho (11)

9 Hukumu za Mungu haziepekiki (1-10)
Kibanda cha Daudi kitainuliwa (11-15)

1 Maneno ya Amosi,* aliye-kuwa mmoja wa wafugaji wa kondoo kutoka Tekoa,^a ali-yoyapokea katika maono kuhusu Israeli katika siku za utawala wa Mfalme Uzia^b wa Yuda na katika siku za utawala wa Yeroboamu^c mwana wa Yoashi,^d mfalme wa Israeli, miaka miwili kabla ya tetemeko la ardhi.^e **2** Alisema:

“Yehova atanguruma kuto-ka Sayuni,

Naye atapaza sauti yake kutoka Yerusalemu.

Malisho ya wachungaji yataomboleza,

Na kilele cha Karmeli kita-kaui.”^f

3 “Yehova anasema hivi:

“Kwa sababu ya maasi ma-tatu* ya Damasko, na hata manne, sitabadili uamuzi wangu,

Kwa sababu walipura Gi-leadi kwa vifaa vya chu-ma vya kupuria.^g

4 Kwa hiyo nitaishushia moto nyumba ya Ha-zaeli,^h

Nao utateketeza kabisa minara ya Ben-hadadi yenye ngome.ⁱ

5 Nitavunja makomeo ya Damasko;^j

Nitawaangamiza wakaaji wa Bikath-aveni

Na yule anayetawala* Beth-edeni;

Na watu wa Siria watape-lekwa uhamishoni kule Kiri,^k asema Yehova.’

6 Yehova anasema hivi:

“Kwa sababu ya maasi ma-tatu ya Gaza,^l na hata

SURA YA 1

a 2Nya 11:5, 6

b 2Nya 26:1, 3, 4
Isa 1:1

c 2Fa 14:23, 24
Ho 1:1
Amo 7:10

d 2Fa 13:10, 11

e Zek 14:5

f Isa 33:9
Nah 1:4

g 2Fa 8:12
2Fa 10:32, 33
2Fa 13:7

h 1Fa 19:15

i Yer 49:27

j Isa 7:8
Isa 8:4
Isa 17:1

k 2Fa 16:9

l Eze 25:15

Safu ya 2

a 2Nya 21:16, 17
2Nya 28:18
Yoe 3:4, 6

b Yer 25:17, 20
Yer 47:1
Zek 9:5

c Isa 20:1

d Yer 47:5

e Sef 2:4

f Isa 14:29
Yer 47:4
Eze 25:16, 17
Sef 2:5
Zek 9:6

g Eze 26:2

h Yoe 3:4, 6

i Eze 26:12

j Yoe 3:19

k Eze 25:12

manne, sitabadili uamu-zi wangu,

Kwa sababu walichukua kundi lote la mateka^a na kuwatia mikononi mwa Edomu.

7 Basi nitaushushia moto ukuta wa Gaza,^b

Nao utateketeza kabisa mi-nara yake yenye ngome.

8 Nitawaangamiza wakaaji wa Ashdodi,^c

Na mtawala* wa Ashke-loni;^d

Nitaugeuza mkono wangu dhidi ya Ekroni,^e

Na Wafilisti wanaobaki wa-taangamia,^f asema Bwa-na Mwenye Enzi Kuu Ye-hova.’

9 Yehova anasema hivi:

‘Kwa sababu ya maasi ma-tatu ya Tiro,^g na hata manne, sitabadili uamu-zi wangu,

Kwa sababu walilitia miko-noni mwa Edomu kundi lote la watu waliohami-shwa,

Na kwa sababu hawakuku-mbuka agano la ndugu.^h

10 Basi nitaushushia moto ukuta wa Tiro,

Nao utateketeza kabisa mi-nara yake yenye ngome.’ⁱ

11 Yehova anasema hivi:

‘Kwa sababu ya maasi ma-tatu ya Edomu,^j na hata manne, sitabadili uamu-zi wangu,

Kwa sababu alimfuatia kwa upanga ndugu yake mwenyewe,^k

Na kwa sababu alikataa kuonyesha rehema;

Katika hasira yake ana-endelea kuwaruaruara bila huruma,

1:1 *Maana yake “Kuwa Mzigo” au “Ku-beba Mzigo.” 1:3 *Au “matendo mata-tu ya uhalifu.” 1:5, 8 *Tnn., “yule ana-yeshika fimbo ya ufalme.”

Na bado anaendelea kuwa-
kasirikia vikali.^a

12 Basi nitaishushia moto
Temani,^b

Nao utateketeza kabisa
minara ya Bosra yenye
ngome.^c

13 Yehova anasema hivi:

“Kwa sababu ya maasi ma-
tatu ya Waamoni,^d na
hata manne, sitabadili
uamuzi wangu,

Kwa sababu waliwapasua
tumbo wanawake wenye
mimba wa Gileadi ili
wapanue eneo lao
wenyewe.^e

14 Basi nitaushushia moto
ukuta wa Raba,^f

Nao utateketeza kabisa
ngome zake zenye
minara,

Kwa kelele za vita katika
siku ya mapigano,
Kwa tufani katika siku ya
kimbunga.

15 Na mfalme wao atapele-
kwa uhamishoni pamoja
na wakuu wake,^g asema
Yehova.’

2 “Yehova anasema hivi:

“Kwa sababu ya maasi
matatu* ya Moabu,^h na
hata manne, sitabadili
uamuzi wangu,

Kwa sababu aliiteketeza
mifupa ya mfalme wa
Edomu kwa ajili ya
chokaa.

2 Kwa hiyo nitaishushia
moto Moabu,

Nao utateketeza kabisa mi-
nara ya Keriothi yenye
ngome;ⁱ

Moabu itakufa katika
ghasia,

Kwa kelele za vita, kwa
mlio wa pembe.^j

SURA YA 1

a 2Nya 28:17
Oba 10

b Mwa 36:10, 11
Oba 9

c Isa 34:5, 6
Yer 49:13

d Eze 25:3
Sef 2:8

e Amu 11:12, 13
Yer 49:1

f Yer 49:2
Eze 25:5

g Yer 27:2, 3
Yer 49:3

SURA YA 2

h Yer 48:29, 30
Eze 25:8, 9
Sef 2:8

i Yer 48:21, 24

j Isa 15:1

Safu ya 2

a Isa 16:14
Yer 48:7

b 2Fa 17:19
Yer 2:13

c Law 26:14-16
2Nya 36:14

d Yer 9:14

e 1Sa 12:15
1Nya 28:9
2Nya 36:17, 19
Yer 17:27
Yer 37:8
Yer 52:12-14
Ho 8:14

f Kum 28:45
2Fa 17:6, 7
Eze 23:4, 5
Ho 4:1, 2

g Amo 5:11
Amo 8:4-6

h Amo 4:1

i Isa 10:1, 2
Amo 5:12

j Ho 8:11
Ho 10:1

3 Nitamwondoa mtawala*
miongoni mwake

Na kuwaua wakuu wake
wote pamoja naye,^a ase-
ma Yehova.’

4 Yehova anasema hivi:

‘Kwa sababu ya maasi ma-
tatu ya Yuda,^b na hata
manne, sitabadili uamu-
zi wangu,

Kwa sababu walikataa she-
ria* ya Yehova,

Na kwa sababu hawaku-
fuata masharti yake;^c

Lakini uwongo uleule
ambao mababu zao wali-
fuata umewapotosha.^d

5 Kwa hiyo nitaishushia
moto Yuda,

Nao utateketeza kabisa mi-
nara ya Yerusalemu ye-
nye ngome.^e

6 Yehova anasema hivi:

‘Kwa sababu ya maasi ma-
tatu ya Israeli,^f na hata
manne, sitabadili uamu-
zi wangu,

Kwa sababu wanamuza
mwadilifu ili wapate
fedha,

Na maskini kwa jozi ya
viatu.^g

7 Wanavikanyaga-kanyaga
vichwa vya watu wa hali
ya chini katika mavumbi
ya dunia,^h

Nao wanaziba njia ya
wapole.ⁱ

Mtu na baba yake wanalala
na msichana yuleyule,
Na hivyo kulichafua jina
langu takatifu.

8 Wanajinyoosha kando ya
kila madhabahu/ juu ya
nguo walizochukua kwa
nguvu kutoka kwa ma-

2:3 *Tnn., “mwamuzi.” 2:4 *Au “mafundi-
ndisho.”

2:1 *Au “matendo matatu ya uhalifu.”

skini kama dhamana ya mkopo;*^a

Na divai wanayokunywa katika nyumba ya[#] miungu yao waliipata kutoka kwa wale waliowatoza faini.’

9 ‘Lakini ni mimi niliyemwanamiza Mwamori mbele yao,^b

Aliyekuwa mrefu kama mierezi na mwenye nguvu kama mialoni; Niliyaharibu matunda yake juu na mizizi yake chini.^c

10 Nilikupandisha kutoka nchini Misri,^d

Nami nikakufanya ute-mbee kupitia nyikani kwa miaka 40,^e

Ili umiliki nchi ya Mwamori.

11 Niliwainua baadhi ya wana wako kuwa manabii^f

Na baadhi ya vijana wako wa kiume kuwa Wana-dhiri.^g

Je, sivyo ilivyo, enyi watu wa Israeli?’ asema Yehova.

12 ‘Lakini uliendelea kuwapa Wana-dhiri divai wanywe,^h

Nawe ukawaamuru hivi manabii: “Hampaswi kutoa unabii.”ⁱ

13 Basi nitakupondaponda mahali pako,

Kama vile ambavyo gari la kukokotwa lililojazwa miganda ya nafaka iliyo-toka kuvunwa linavyopondaponda kilicho njiani.

14 Mwenye mbio hatakuwa na mahali pa kukimbilia,^j

2:8 *Au “rehani.” #Au “hekalu la.”

SURA YA 2

a Kut 22:26
Kum 24:12

b Hes 21:23-25
Yos 24:8
Zb 135:10, 11

c Kum 2:31-33

d Kut 12:51

e Hes 14:34
Kum 2:7

f 1Sa 3:20
1Fa 17:1
1Fa 19:19

g Hes 6:2
Amu 13:5

h Hes 6:3, 4

i Isa 30:10, 11
Amo 7:12, 13

j Amo 9:1

Safu ya 2

a Kum 28:25

SURA YA 3

b Kut 19:5
Kum 7:6
Zb 147:19, 20

c Da 9:11, 12
Ho 12:2
Amo 4:12

Mwenye nguvu hatabaki na nguvu zake, Na hakuna shujaa atakayeokoa uhai wake.*

15 Mwanamume anayeshika upinde hatasimama, Mtu anayekimbia kwa kasi[#] hataponyoka, Na mpanda farasi hataokoa uhai wake.*

16 Hata mashujaa wenye ujaisiri* zaidi Watakimbia uchi siku hiyo,^a asema Yehova.”

3 “Sikieni neno hili ambalo Yehova amesema kuwahu-su ninyi, enyi watu wa Israeli, kuhusu familia nzima niliyoi-pandisha kutoka nchini Misri:

2 ‘Ni ninyi peke yenu niliowajua kati ya familia zote duniani.^b

Ndiyo sababu nitawafanya muwajibike* kwa sababu ya makosa yenu yote.^c

3 Je, watu wawili watatemeba pamoja ikiwa hawajakubaliana kuku-tana?*

4 Je, simba atanguruma mwituni ikiwa hana mawindo?

Je, mwanasimba* atanguruma pangoni mwa-ke ikiwa hajakamata chochote?

5 Je, ndege ataanguka kwenye mtego ardhini ikiwa hakuna mtego wa kuhakuna?*

2:14, 15 *Au “nafsi yake.” 2:15 #Tnn., “mwenye miguu myepesi.” 2:16 *Au “wenye moyo mkuu.” 3:2 *Au “nitawaadhibu.” 3:3 *Au “hawajakutana kama walivyokubaliana.” 3:4 *Au “mwanasimba mwenye manyoya marefu shingoni.” 3:5 *Au labda, “ikiwa hauna chambo?”

Je, mtego hufyatuka ardhini ikiwa haujanasa chochote?

- 6** Pembe ikipigwa jijini, je, watu hawatetemeki? Msiba ukitokea jijini, je, si Yehova aliyetenda?
- 7** Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova hatafanya jambo lolote Kabla hajawafunulia watu-mishi wake manabii siri yake.^a
- 8** Simba amenguruma!^b Ni nani ambaye hataogopa? Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema! Ni nani ambaye hatatoa unabii?^c
- 9** ‘Tangazeni jambo hilo kwenye minara ya Ashdodi yenye ngome Na kwenye minara yenye ngome katika nchi ya Misri. Semeni: “Kusanyikeni pamoja dhidi ya milima ya Samaria;^d Tazameni machafuko yaliyo ndani yake.^e
- 10** Kwa maana hawajui kufanya yaliyo sawa,” asema Yehova, “Wale wanaojikusanyia ukatili na maangamizi katika minara yao yenye ngome.”
- 11** Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi: ‘Adui ataizingira nchi,^f Atakuvua nguvu zako, Na minara yako yenye ngome itaporwa.’^g
- 12** Yehova anasema hivi: ‘Kama mchungaji anavyompokonya simba miguu

SURA YA 3

a Mwa 6:13
Mwa 18:17
Zb 25:14
Isa 42:9
Da 9:22
Ufu 1:1

b Amo 1:2

c Yer 20:9
Amo 7:14, 15
Mdo 4:19, 20

d 2Fa 17:22, 23

e Ho 7:1
Amo 4:1

f 2Fa 17:6

g Ho 11:6
Amo 6:8

Safu ya 2

a Isa 8:4
Amo 6:4

b Ho 4:9

c 1Fa 12:32, 33
Ho 13:2

d 2Fa 23:15, 16
2Nya 31:1
2Nya 34:1, 7
Ho 10:2
Mik 1:6

e 1Fa 22:39

f Amo 6:11

SURA YA 4

g Amo 6:1

h Ho 4:1, 2
Mik 2:2

miwili au kipande cha sikio kutoka kinywani mwake,

Hivyo ndivyo watu wa Israeli watakavyookolewa,

Wale ambao sasa wanaketi kwenye vitanda vya kifahari na kwenye makochi bora* kule Samaria.^a

- 13** ‘Sikieni na kuionya* nyumba ya Yakobo,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, Mungu wa majeshi.

14 ‘Kwa maana siku nitakapowafanya Waisraeli wawajibike* kwa sababu ya maasi yao yote,^{#b}

Pia nitawafanya wawajibike kwa sababu ya madhabahu za Betheli;^c

Pembe za madhabahu zitatakwa na kuanguka ardhini.^d

- 15** Nitaibomoa nyumba ya majira ya baridi kali pamoja na nyumba ya majira ya kiangazi.’

‘Nyumba za pembe za tembo zitatoweka,^e

Na majumba makubwa hayatasalia,^{**f} asema Yehova.”

4 “Sikieni neno hili, enyi ng’ombe wa Bashani, Mlio kwenye mlima wa Samaria,^g

Ninyi wanawake mnaowalaghai watu wa hali ya chini^h na kuwakandamiza maskini,

Mnaowaambia waume

3:12 *Au “makochi ya Damasko.” **3:13** *Au “kutoa ushahidi dhidi ya.”

3:14 *Au “nitakapowaadhibu Waisraeli.” [#]Au “matendo yao yote ya uhalifu.”

3:15 *Au labda, “nyumba nyingi hazitasalia.”

zenu,* ‘Tuleteeni kinywaji!’

2 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ameapa kwa utakatifu wake,

“‘Tazameni! Siku zinakuja wakati ambapo atawainua juu kwa kulabu za mchinjaji wa wanyama Na wale watakaobaki kati yenu kwa ndoano za samaki.

3 Kila mmoja wenu atatoka nje moja kwa moja kupitia sehemu zilizobomolewa ukutani;

Nanyi mtatupwa kule Harmoni,” asema Yehova.’

4 ‘Njoooni Betheli mtende dhambi,*^a

Njoooni Gilgali mzidi kute ndani dhambi!^b

Leteni dhabihu zenu^c asubuhi,

Na sehemu zenu za kumi^d katika siku ya tatu.

5 Teketezeni dhabihu ya shukrani ya mikate ili-yotiwa chachu;^e

Tangazeni kwa sauti matoleo yenu ya hiari!

Kwa maana hivyo ndivyo mnavyopenda kufanya, enyi watu wa Israeli,’ asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

6 ‘Lakini mimi niliyafanya meno yenu yawe safi bila chakula* katika majiji yenu yote

Nikasababisha mkose mikate katika nyumba zenu zote;^f

Lakini hamkunirudia,^g asema Yehova.

4:1 *Au “mabwana wenu wakubwa.”
4:4 *Au “mfanye uasi.” 4:6 *Au “sikuwapa chakula chochote.”

SURA YA 4

a 1Fa 12:28, 29
Ho 4:13
Amo 3:14

b Ho 4:15
Ho 9:15
Amo 5:5

c Ho 8:11, 13

d Kum 14:28

e Law 7:12

f Law 26:26
Kum 28:38
Kum 32:24
1Fa 18:2
2Fa 4:38

g Yer 3:6, 7

Safu ya 2

a Kum 28:23, 24

b 1Fa 18:5

c Ho 7:10

d Kum 28:22

e Kum 28:40, 42

f Isa 42:24

g Kut 9:3
Kum 28:27, 60

h Law 26:23, 25
2Fa 8:12

i 2Fa 13:7

j Kum 28:26

k Mwa 19:24, 25

l Ho 7:10

7 ‘Pia niliwanyima mvua miezi mitatu kabla ya mavuno;^a

Nilileta mvua katika jiji moja lakini sikuileta katika jiji lingine.

Shamba moja lilipata mvua,

Lakini shamba lingine lilikauka kwa sababu halikupata mvua.

8 Watu wa majiji mawili au matatu walipepesuka kwenda kwenye jiji moja kunywa maji,^b

Nao hawakutosheka; Lakini hamkunirudia,^c asema Yehova.

9 ‘Niliwapiga kwa joto linalounguza na kuvu.^d

Mlizardisha bustani zenu na mashamba yenu ya mizabibu,

Lakini nzige walitafuna mitini yenu na mizeituni yenu;^e

Na bado hamkunirudia,^f asema Yehova.

10 ‘Niliwaleta ugonjwa hata-ri kama ule wa* Misri.^g

Niliwaua vijana wenu wa kiume^h kwa upanga na kuwateka farasi wenu.ⁱ

Nilifanya uvundo wa kambi zenu upande katika mianzi ya pua zenu;^j

Lakini hamkunirudia,’ asema Yehova.

11 ‘Niliwaangamiza Kama Mungu alivyoa-ngamiza Sodoma na Gomora.^k

Nanyi mlikuwa kama gogo lililochomolewa haraka motoni;

Lakini hamkunirudia,^l asema Yehova.

4:10 *Au “tauni kama ile ya.”

12 Basi hivyo ndivyo nitakavyokutendea, Ee Israeli. Kwa kuwa nitakutendea hivyo,

Jitayarisha kukutana na Mungu wako, Ee Israeli.

13 Kwa maana tazama! yeye Ndiye aliyumba milima^a na kuumba upepo;^b

Humwambia mwanadamu mawazo Yake,

Hubadili mapambazuko kuwa giza,^c

Naye hukanyaga vilele vya dunia;^d

Yehova Mungu wa majeshi ndilo jina lake.”

5 “Sikieni neno hili ninalosema dhidi yenu kama wimbo wa huzuni,* Ee nyumba ya Israeli:

2 ‘Bikira, Israeli, ameanguna;

Hawezi kuinuka tena.

Ameachwa peke yake katika ardhi yake mwenyewe;

Hakuna yeyote wa kumwina.’

3 “Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova anasema hivi:

‘Jiji linaloenda vitani likiwa na watu elfu moja litabaki na watu mia moja; Na lile linaloenda vitani na watu mia moja litabaki na watu kumi, hili linahusu nyumba ya Israeli.’^e

4 “Kwa maana Yehova anaambia hivi nyumba ya Israeli: ‘Nitafuteni mimi mwendelee kuishi.’^f

5 Msitafute Betheli,^g Msiende Gilgali^h wala

5:1 *Au “wimbo wa maombolezo.”

SURA YA 4

a Isa 40:12

b Yer 10:13

c Kut 10:22
Isa 5:30
Amo 8:9

d Mik 1:3

SURA YA 5

e Kum 4:27
Kum 28:62

f 2Nya 15:2
Isa 55:3, 6

g 1Fa 12:28, 29
Amo 3:14

h Ho 4:15
Amo 4:4

Safu ya 2

a Amo 8:14

b 2Fa 17:6
Ho 9:15

c Eze 33:11

d Amo 6:12

e Ayu 9:9
Ayu 38:31-33

f Kut 10:21, 22

g Ayu 36:27, 28
Mhu 1:7

h 1Fa 18:17
1Fa 22:8

msivuke kwenda Beer-sheba,^a

Kwa maana Gilgali hakika litapelekwa uhamishoni,^b

Na Betheli litaangamizwa.*

6 Mtafuteni Yehova, mwendelee kuishi,^c

Ili asilipuke kama moto kwenye nyumba ya Yosefu,

Na kuteketeza kabisa Betheli, hivi kwamba haku-na mtu atakayeweza kuuzima moto huo.

7 Mabadili haki kuwa pakanga,^{*}

Nanyi mnautupa uadilifu ardhini.^d

8 Yule aliyumba kundi la nyota la Kima* na kundi la nyota la Kesili,^{#e}

Yule anayebadili kivuli kizito kuwa asubuhi,

Yule anayefanya mchana uwe na giza kama usiku,^f

Yule anayeyaita maji ya bahari

Ili ayamwage kwenye nchi kavu^g

—Yehova ndilo jina lake.

9 Atasababisha maangamizi yawajie kwa ghafla wenyenguvu,

Na kuharibu ngome.

10 Wanawachukia wale wanaotoa karipio kwenye lango la jiji,

Na kuwachukia sana watu wanaosema ukweli.^h

11 Kwa sababu mnamdai maskini kodi ya* shamba

5:5 *Au labda, “litakuwa kitu cha uchiwi.” 5:7 *Au “uchungu.” 5:8 *Labda ni nyota zinazoitwa Pleiadesi katika kundi la nyota la Taurusi, au Ng’ombe. #Labda ni kundi la nyota la Orioni. 5:11 *Au “ushuru wa.”

Nanyi mnachukua nafaka yake kama ushuru,^a

Hamtaendelea kuishi katika nyumba mlizojenga kwa mawe yaliyocho-ngwa^b

Wala hamtakunywa divai kutoka katika mashamba bora ya mizabibu mliyopanda.^c

- 12** Kwa maana ninajua jinsi maasi yenu* yalivyo mengi

Na jinsi dhambi zenu zilivyo kubwa

—Mnawanyanyasa waadilifu,

Mnapokea rushwa,[#]

Nanyi mnawanyima maskini haki zao kwenye lango la jiji.^d

- 13** Kwa hiyo, wale walio na ufahamu watanyamaza kimya wakati huo, Kwa sababu utakuwa wakati wa msiba.^e

- 14** Tafuteni yaliyo mema, na wala si maovu,^f

Ili mwendelee kuishi.^g

Ndipo huenda Yehova Mungu wa majeshi atakuwa pamoja nanyi,

Kama mnavyosema yuko pamoja nanyi.^h

- 15** Chukieni maovu, pendeni yaliyo mema,ⁱ

Acheni haki itawale kwenye lango la jiji.^j

Huenda Yehova Mungu wa majeshi

Atawaonyesha kibali wazao waliobaki wa Yosefu.^k

- 16** “Kwa hiyo Yehova Mungu wa majeshi, Yehova, anasema hivi:

5:12 *Au “matendo yenu ya uhalifu.”
#Au “hongo.”

SURA YA 5

a Mik 2:2

b Isa 9:9, 10

c Kum 28:30

d Isa 10:1, 2
Amo 2:6, 7

e Mik 2:3

f Isa 1:16, 17
Mik 6:8

g Law 18:5
Kum 30:19, 20

h 2Nya 15:2
Mik 3:11

i Zb 34:14
Zb 97:10
Ro 12:9

j 2Nya 19:6
Amo 5:24

k Yer 31:7
Zek 10:6

Safu ya 2

a Ho 9:2

b Isa 5:18, 19

c Amo 4:12

d Sef 1:14, 15

e Met 15:8

f Zb 50:8
Isa 66:3
Ho 6:6

g Isa 1:11

‘Watu watalia kwa sauti katika viwanja vyote vya jiji,

Katika barabara zote wata sema, “Ole! Ole!”

Watawaita wakulima waomboleze

Na waombolezaji wa kulipwa walie kwa sauti.’

- 17** ‘Kutakuwa na kilio katika kila shamba la mizabibu,^a

Kwa maana nitapita katikati yenu,’ asema Yehova.

- 18** ‘Ole wao wanaoitamani siku ya Yehova!^b

Basi, siku ya Yehova itamaanisha nini kwenu?^c

Itakuwa giza, wala si nuru.^d

- 19** Itakuwa kama mtu anayemkimbia simba, kisha anakutana na dubu,

Na anapoingia nyumbani mwake na kuuegemeza mkono wake ukutani, anaumwa na nyoka.

- 20** Je, siku ya Yehova haitakuwa giza, wala si nuru; Je, haitakuwa na utusitusi, wala si mwangaza?

- 21** Nazichukia, nazidharau sherehe zenu,^e

Nami sifurahii harufu tamu ya makusanyiko yenu matakatifu.

- 22** Hata mkinitolea dhahihu nzima za kuteketezwa na matoleo ya zawadi, Sitazifurahia;^f

Nami sitapendezwa na dhahihu zenu za ushirika za wanyama walioneshwa.^g

- 23** Niondoleeni kelele za nyimbo zenu;

Na sitaki kusikia miziki ya vinanda vyenu.^a

24 Acheni haki itiririke kama maji,^b

Na uadilifu kama kijito kinachotiririka daima.

25 Je, uliniletea dhahibu na matoleo ya zawadi

Kwa miaka 40 uliyokuwa nyikani, Ee nyumba ya Israeli?^c

26 Sasa mtalazimika kumchukua Sakuthi mfalme wenu na Kaiwani,*

Sanamu zenu, nyota ya mungu wenu ambaye mlilitengenezea,

27 Nami nitawapeleka uhamishoni mbali kupita Damasko,^d anasema yeye ambaye jina lake ni Yehova Mungu wa majeshi.^e

6 “Ole wao wanaojitumaini* huko Sayuni,

Wale wanaojiona wakiwa salama katika mlima wa Samaria,^f

Wanaume maarufu wa taifa kuu zaidi kati ya mataifa,

Wale ambao nyumba ya Israeli hawaendea!

2 Vukeni mwende Kalne mkaone.

Tokeni huko mwende katika Jiji Kubwa la Hamathi,^g

Na mteremke mpaka jiji la Gathi la Wafilisti.

Je, majiji hayo ni bora kuliko falme hizi,*

Au je, eneo lao ni kubwa kuliko lenu?

5:26 *Huenda miungu hiyo miwili inarejelea sayari ya Zohali, ambayo iliabudiwa kama mungu. 6:1 *Au “wasiojali.” 6:2 *Inaonekana falme hizo ni Yuda na Israeli.

SURA YA 5

a Amo 6:5
Amo 8:10

b Mik 6:8

c Mdo 7:42, 43

d 2Fa 15:29
2Fa 17:6

e Amo 4:13

SURA YA 6

f Amo 3:13, 15

g Hes 34:2, 8
2Fa 14:28

Safu ya 2

a Isa 56:12

b Amo 5:12

c 1Fa 22:39

d Amo 3:12

e Isa 22:13

f Isa 5:12

g 2Nya 7:6
2Nya 29:25, 26

h Isa 5:11

i 2Fa 15:29
2Fa 17:6

j Kum 28:41
Amo 5:5

k Amo 4:2

l Eze 33:28
Ho 5:5

m Omb 2:5

n Mik 1:6

3 Je, mnaiondoa akilini mwenu ile siku ya msiba^a Na kuukaribisha utawala wa* ukatili?^b

4 Wanalalia vitanda vya pembe za tembo^c na kuji-nyoosha kwenye makochi,^d

Wakila kondoo dume wa kundi na ndama* waliononeshwa;^e

5 Wanatunga nyimbo papo hapo kupatana na sauti ya kinubi,^f

Na kama Daudi, wanabuni ala za muziki;^g

6 Wanakunywa divai iliyojizwa kwenye mabakuli^h Na kujitia wenyewe mafuta yaliyo bora.

Lakini hawajali* msiba wa Yosefu.ⁱ

7 Basi watakuwa mstari wa mbele kupelekwa uhamishoni,^j

Na karamu zenye shamrashamra za wanaojinyoosha kwa starehe zitakoma.

8 ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ameapa kwa nafsi yake mwenyewe,^k asema Yehova Mungu wa majeshi,

“Nakichukia sana kiburi cha Yakobo,^l

Naichukia minara yake yenye ngome,^m

Nami nitawapa wengine jiji lao na vyote vilivyomo.ⁿ

9 ““Na watu kumi wakibaki katika nyumba moja, wao pia watakufa. 10 Mtu wa ukoo*
6:3 *Tnn., “kukikaribisha kiti cha.” 6:4 *Au “ng’ombe dume wachanga.” 6:5 *Au “kinanda.” 6:6 *Tnn., “hawakuwa wagonjwa kwa sababu ya.” 6:10 *Tnn., “Ndugu ya baba yake.”

atakuja na kuwatoa nje na kuwachoma mmoja baada ya mwingine. Ataitoa mifupa yao ndani ya nyumba hiyo; kisha atamuuliza yeyote aliye katika vyumba vya ndani vya nyumba hiyo, 'Je, kuna wengine pamoja nawe?' Naye atajibu, 'Hakuna yeyote!' Kisha atasema, 'Nyamaza kimya! Kwa maana huu si wakati wa kutaja kwa vyovyote vile jina la Yehova.'"

11 Kwa maana ni Yehova anayetoa amri hiyo,^a

Naye ataibomoa ile nyumba kubwa ibaki rundo la mawe,

Na nyumba ndogo ibaki kifusi.^b

12 Je, farasi hukimbia kwenye mwamba,

Au je, mtu anaweza kulima kwa ng'ombe kwenye mwamba?

Kwa maana mmebadili haki kuwa mmea wenye sumu,

Na tunda la uadilifu kuwa pakanga.*^c

13 Mnashangilia jambo lisilo na manufaa yoyote,

Nanyi mnasema, "Je, hatu-japata nguvu* kwa uwezo wetu wenyewe?"^d

14 Kwa hiyo, Ee nyumba ya Israeli, nitaleta taifa dhidi yenu,^e asema Yehova Mungu wa majeshi,

'Nalo litawakandamiza kuanzia Lebo-hamathi^f mpaka kwenye Korongo^Δ la Araba.'"

6:12 *Au "uchungu." 6:13 *Tnn., "hatakujitwalia pembe." 6:14 *Au "njia ya kuingia Hamathi." ^Δ Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 6

a Isa 10:5, 6

b Amo 3:15

c 1Fa 21:13
Isa 59:13
Ho 10:4
Amo 5:7d Kum 8:17, 18
Zb 75:5e Kum 28:49, 50
2Fa 15:29
2Fa 17:6
Isa 7:20
Isa 8:4
Isa 10:5, 6
Ho 10:6

f Hes 34:2, 8

Safu ya 2

SURA YA 7

a Yer 14:7
Da 9:19

b Isa 37:4

c Kum 32:36
Zb 106:44, 45
Ho 11:8

d Kut 32:11

e Isa 1:9
Amo 7:2

f Kut 32:14

g Amo 8:2

7 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alinionyesha mambo haya: Tazama! Alileta kundi la nzige mimea ya mwisho* ilipokuwa ikianza kuchi-puka. Mimea hiyo ilipandwa baada ya nyasi za mfalme kukatwa. **2** Kundi hilo la nzige lilipomaliza kula mimea nchini, nikasema: "Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, tafadhali samehe!^a Yakobo atae-ndeleaje kuishi?"* Kwa maana yuko dhaifu!"^b

3 Basi Yehova akafikiria upya* jambo hilo.^c Yehova akasema, "Hilo halitatokea."

4 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alinionyesha mambo haya: Tazama! Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova aliamuru moto uje kuwaadhibu. Uka-teketeza vilindi vikubwa vya maji, na kuteketeza sehemu ya nchi. **5** Kisha nikasema: "Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, tafadhali lizuie jambo hili lisitendeke.^d Yakobo atae-ndeleaje kuishi?"* Kwa maana yuko dhaifu!"^e

6 Basi Yehova akafikiria upya* jambo hilo.^f Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova akasema, "Hilo pia halitatokea."

7 Alinionyesha mambo haya: Tazama! Yehova alikuwa amesimama juu ya ukuta uliojengwa kwa timazi,* na timazi ilikuwa mkononi mwake. **8** Kisha Yehova akaniuliza: "Unaona nini, Amosi?" Nikamjibu: "Timazi." Ndiipo Yehova akasema: "Tazama na-weka timazi kati ya watu wangu Waisraeli. Sitawasamehe tena."^g **9** Sehemu za juu

7:1 *Yaani, mwezi wa Januari na Februari. 7:2, 5 *Tnn., "atainukaje?" 7:3, 6 *Au "akaghairi kuhusu." 7:7 *Au "chubwi; bildi."

za Isaka^a zitaachwa ukiwa, na mahali patakatifu pa Waisraeli pataharibiwa kabisa;^b nami ni-taishambulia nyumba ya Yero-boamu kwa upanga.”^c

10 Kuhani Amazia wa Betheli^d akatuma ujumbe huu kwa Mfalme Yeroboamu^e wa Israeli: “Amosi anapanga njama dhidi yako katikati kabisa ya nyumba ya Israeli.^f Nchi haiwezi kuvumilia mane-no yake yote.^g **11** Kwa maana Amosi anasema hivi: ‘Yero-boamu atauawa kwa upanga; na kwa hakika Waisraeli watapelekwa uhamishoni kutoka katika nchi yao.’”^h

12 Kisha Amazia akamwambia Amosi: “Ee mwonaji, nenda, kimbia uende katika nchi ya Yuda, jitafutie mkate wako* huko, nawe unaweza kutoa unabii wako huko.ⁱ **13** Lakini usiendeleo kutoa unabii hapa Betheli,^j kwa maana ni mahali patakatifu pa mfalme^k na nyumba ya ufalme.”

14 Ndipo Amosi akamjibu hivi Amazia: “Mimi sikuwa nabii wala mwana wa nabii; bali nilikuwa mchungaji wa mifugo,^l nami nilitunza mitini ya mikuyu.* **15** Lakini Yehova aliniondoa katika kazi ya kuchunga kundi, kisha Yehova akaniambia, ‘Nenda, toa unabii kwa watu wangu Waisraeli.’”^m **16** Basi sasa sikia neno la Yehova: ‘Wewe unasema: “Usitoe unabii dhidi ya Israeli,ⁿ na usihubiri^o dhidi ya nyumba ya Isaka.” **17** Kwa hiyo Yehova anasema hivi: “Mke wako atakuwa kahaba jijini, na wana wako na mabinti wako watauawa kwa upanga.

7:12 *Au “kula mkate.” 7:14 *Au “nili-
chanja tini za mikuyu.”

SURA YA 7

a 1Fa 12:25, 31
1Fa 13:33

b Ho 10:8
Amo 5:5
Amo 8:14

c 2Fa 15:8, 10
Ho 13:16

d 1Fa 12:32

e 2Fa 14:23

f Yer 26:8, 9
Amo 1:1

g Yer 18:18

h Amo 5:5
Amo 6:7

i Isa 30:10

j Amo 2:12

k 1Fa 12:29, 32
1Fa 13:1

l Amo 1:1

m Yer 1:7
Eze 2:3
2Pe 1:21

n Yer 11:21
Amo 7:13

o Mik 2:6

Safu ya 2

a Law 26:33
2Fa 17:6

SURA YA 8

b Amo 4:12
Amo 7:8

c Ho 10:5
Amo 5:23

d Amo 6:9, 10

e Amo 2:6, 7

f Hes 10:10

g Kut 20:8

h Law 19:35, 36
Ho 12:7
Mik 6:10, 11

i Law 25:39
Amo 2:6

Ardhi yako itagawanywa kwa wengine kwa kamba ya kupi-mia, na wewe mwenyewe utafia katika nchi isiyoyafu; na kwa hakika Waisraeli watapelekwa uhamishoni kutoka katika nchi yao.””^a

8 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alinionyesha mambo haya: Tazama! Kulikuwa na kikapu chenye matunda ya wakati wa kiangazi. **2** Kisha akaniuliza, “Unaona nini, Amosi?” Nikajibu, “Kikapu chenye matunda ya wakati wa kiangazi.” Kisha Yehova akaniambia: “Mwisho wa watu wangu Waisraeli umefika. Sitawasamehe tena.^b **3** ‘Siku hiyo nyimbo za hekalu zitabadilika kuwa kilio kikubwa,’^c asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. ‘Kutakuwa na mizoga mingi iliyotupwa kila mahali^d—kimya cha ajabu!’

4 Sikieni hili, ninyi mnao-wakandamiza maskini Na kuwaangamiza wapole nchini,^e

5 Mnaosema, ‘Sherehe ya mwezi mpya itakwisha lini,^f ili tuuze nafaka yetu,

Na Sabato^g itakwisha lini, tukauze nafaka?

Ili tupunguze kipimo cha efa*^h

Na kuongeza uzito wa shekeli,ⁱ

Kuipotisha mizani yetu ya udanganyifu;^h

6 Ili tuwanunue wenye uhitaji kwa fedha

Na maskini kwa jozi ya viatu,ⁱ

Na kuuza makapi ya nafaka.’

8:5 *Angalia Nyongeza B14.

- 7 Yehova ameapa kwa Fahari ya Yakobo,^a
‘Sitasahau kamwe mate-
ndo yao yote.^b
- 8 Kwa sababu hiyo nchi* ita-
tetemeka,
Na kila mkaaji nchini atao-
mboleza.^c
Je, nchi yote haitapanda
kama Mto Nile,
Na kuinuka na kushuka
chini kama Mto Nile wa
Misri?’^d
- 9 ‘Siku hiyo,’ asema
Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova,
‘Nitalifanya jua litue waka-
ti wa adhuhuri,
Nami nitaitia nchi giza
siku nyangavu.’^e
- 10 Nitabadili sherehe zenu
ziwe maombolezo^f
Na nyimbo zenu zote ziwe
nyimbo za huzuni.*
Nitavisha nyonga zote
nguo za magunia na ku-
kitia kila kichwa upara;
Nitafanya wakati huo uwe
kama wakati wa kumwo-
mbolezea mwana wa
pekee,
Na mwisho wake kama
siku yenye uchungu.’
- 11 ‘Tazama! Siku zinakuja,’
asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova,
‘Nitakapoleta njaa kali
nchini,
Si njaa kali ya chakula* au
kiu ya maji,
Bali ya kusikia maneno ya
Yehova.’^g
- 12 Watapepesuka kutoka ba-
hari mpaka bahari
Na kutoka kaskazini mpa-
ka mashariki.*

8:8 *Au “dunia.” 8:10 *Au “maombolezo.” 8:11 *Tnn., “mkate.” 8:12 *Au “mawilo ya jua.”

SURA YA 8

a Kum 33:26
Zb 68:34

b Ho 8:13

c Ho 4:3

d Amo 9:5

e Mik 3:6

f Ho 2:11

g Zb 74:9
Eze 7:26
Mt 4:4

Safu ya 2

a Ho 8:5
Ho 10:5

b 1Fa 12:28-30

c Amo 5:5

d 2Fa 18:11
Ho 13:16

SURA YA 9

e Isa 6:1
Eze 1:27, 28

f Amo 2:14

g Yer 23:24

Watatanganga wakitafu-
ta neno la Yehova, lakini
hawatalipata.

- 13 Siku hiyo mabikira ware-
mbo watazimia,
Na pia vijana wa kiume,
kwa sababu ya kiu;
- 14 Wale wanaoapa kwa hatia
ya Samaria^a na kusema,
“Kwa hakika kama mungu
wako anavyoishi, Ee
Dani!”^b
Na, “Kwa hakika kama
inavyoishi njia ya Beer-
sheba!”^c
Wataanguka, na hawatai-
nuka tena.”^d

9 Nilimwona Yehova^e akiwa
juu ya madhabahu, naye
akasema: “Piga kichwa cha
nguzo, na vizingiti vitatiki-
sika. Kata vichwa vya ngu-
zo, nami nitamuua wa mwisho
kwa upanga. Hakuna yeyote
anayekimbia atakayeponyoka,
na hakuna yeyote anayejaribu
kutoroka atakayefanikiwa.”^f

- 2 Wakichimba chini kuingia
Kaburini,*
Mkono wangu utawatoa
humo;
Na wakipanda juu mbi-
nguni,
Nitawashusha chini kuto-
ka huko.
- 3 Nao wakijificha kwenye
kilele cha Karmeli,
Nitawasaka na kuwatoa
huko.^g
Wakijificha chini ya bahari
ili macho yangu yasi-
waone,
Huko nitamwamuru nyoka
awaume.
- 4 Wakipelekwa utekwani na
maadui wao,

9:2 *Au “Sheoli.” Angalia Kamusi,
uku. 2012.

Huko nitauamuru upanga,
nao utawaua;^a
Nitawakazia macho kwa
mabaya, wala si kwa
mema.^b

- 5 Kwa maana Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu, Yehova wa
majeshi, Ndiye anayeigu-
sa nchi,*

Hivi kwamba inayeyuka,^c
na wakaaji wake wote
wataomboleza;^d

Na nchi yote itapanda
kama Mto Nile,
Na kushuka chini kama
Mto Nile wa Misri.^e

- 6 'Yule anayejenga ngazi
zake mbinguni
Na kujenga jengo* lake juu
ya dunia;

Yule anayeyaita maji ya
bahari,

Ili ayamwage duniani^f
—Yehova ndilo jina lake.^g

- 7 'Je, ninyi si kama wana wa
Wakushi kwangu, enyi
watu wa Israeli?' asema
Yehova.

'Je, sikuwapandisha Wa-
israeli kutoka nchini
Misri,^h

Na Wafilisti kutoka Krete,ⁱ
na Wasiria kutoka Kiri?'

- 8 'Tazameni! Macho ya Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova
yanautazama ufal-
me huu wenye dhambi,
Naye atauangamiza kabisa
kutoka nchini.^k

Lakini sitaiangamiza kabi-
sa nyumba ya Yakobo,^l
asema Yehova.

- 9 'Kwa maana tazameni! Ni-
natoa amri,
Nami nitaichekecha nyu-
mba ya Israeli miongoni
mwa mataifa yote,^m

SURA YA 9

a Law 26:33

b Kum 28:63, 65

c Mik 1:4

d Ho 4:3

e Amo 8:8

f Ayu 36:27, 28
Zb 135:7

g Kut 3:15
Amo 4:13
Amo 5:8

h Kut 12:51

i Yer 47:4

j 2Fa 16:9

k 1Fa 13:34
2Fa 18:11

l Yer 30:11

m Law 26:33
Kum 28:64

Safu ya 2

a Isa 9:6, 7
Isa 16:5
Yer 23:5
Eze 37:24, 25
Zek 12:8
Lu 1:31-33

b 2Sa 7:11
Mdo 15:16-18

c Hes 24:18
Isa 11:14
Oba 18, 19

d Law 26:5
Ho 2:22

e Yoe 3:18

f Isa 35:1
Isa 55:12

g Ezr 3:1
Yer 30:3
Eze 39:25

h Isa 61:4
Eze 36:33

Kama mtu anavyocheke-
cha nafaka kwa chujio,
Na hakuna kijiwe hata
kimoja kinachoanguka
chini.

- 10 Watu wangu wote wanao-
tenda dhambi watauawa
kwa upanga,

Wale wanaosema: "Msiba
hautatukaribia wala ku-
tufikia."

- 11 'Siku hiyo nitakiinua kiba-
nda cha Daudi^a kilichoan-
guka,*

Nitarekebisha sehemu[#] zi-
lizoharibika,

Na kujenga upya magofu
yake;

Nitakijenga upya kama ki-
livyokuwa siku za kale,^b

- 12 Ili wamiliki sehemu zilizo-
baki za Edomu,^c

Na mataifa yote yanayoi-
twa kwa jina langu,' ase-
ma Yehova, anayefanya
hayo.

- 13 'Tazameni! Siku zinakuja,[']
asema Yehova,

'Wakati ambapo mtu ana-
yelima kwa plau atampi-
ta anayevuna,

Na anayekanyaga zabibu
atampita anayepanda
mbegu,^d

Na milima itadondosha
divai tamu,^e

Na vilima vyote vitatiriri-
ka divai.^{*f}

- 14 Nitawakusanya na kuwa-
rudisha watu wangu Wa-
israeli walio utekwani,^g
Nao watajenga upya majiji
yaliyoachwa ukiwa na
kuishi humo;^h

9:11 *Au "hema la Daudi lililoanguka."
#Au "sehemu zao." 9:13 *Tnn., "vitaye-
yuka."

Watapanda mashamba ya
mizabibu na kunywa di-
vai yake,^a

Nao watalima bustani za
matunda na kula matu-
nda yake.^b

SURA YA 9

a Isa 65:21, 22
Eze 28:25, 26
b Isa 62:8, 9
Mik 4:4

Safu ya 2

a Isa 60:21
Eze 34:27, 28
Eze 37:25

15 'Nitawapanda katika nchi
yao,
Nao hawatang'olewa tena
kamwe
Kutoka katika nchi yao
ambayo nimewapa,^a ase-
ma Yehova Mungu wenu."

OBADIA

YALIYOMO

Kunyenyekeswa kwa taifa la Edomu
lenye kiburi (1-9)
Taifa la Edomu lamtendea Yakobo
ukatili (10-14)
Siku ya Yehova ya kuhukumu mataifa
yote (15, 16)

Kurudishwa kwa nyumba ya
Yakobo (17-21)
Edomu kuangamizwa na Yakobo (18)
Ufalme utakuwa wa Yehova (21)

1 Maono ya Obadia:*

Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova anasema hivi ku-
husu Edomu:^a

"Tumesikia habari kutoka
kwa Yehova,
Mjumbe ametumwa kati ya
mataifa:

'Inukeni, tujitayarisha ku-
pigana na Edomu."^b

2 "Tazama! Nimekufanya
uwe mdogo sana kati ya
mataifa;

Unadharauliwa kabisa.^c

3 Kimbelebele cha moyo
wako kimekudanganya,^d
Wewe unayeishi katika ma-
pango ya mwamba,
Unayekaa juu, ukisema
moyoni mwako,
'Ni nani atakayenishusha
chini duniani?'

a Isa 21:11
Eze 25:12-14
Yoe 3:19
Amo 1:11, 12

b Yer 49:14-16

c Yer 49:8

d Mal 1:4

Safu ya 2

a Kum 24:21
Yer 49:9, 10

4 Hata ukijenga makao yako
juu* kama tai,
Au ukiweka kiota chako
kati ya nyota,
Nitakushusha chini kutoka
huko," asema Yehova.

5 "Ikiwa wezi wangekuva-
mia, ikiwa wanyang'anyi
wangekuja usiku,
Je, hawangeiba tu wana-
chotaka?

Au ikiwa wavunaji wa zabi-
bu wangekuja kwako,
Je, hawangeacha zabibu
chache?

Lakini wewe utaangami-
zwa kabisa!^a

6 Lo! Jinsi ambavyo Esau
ametafutwa!

Jinsi hazina zake zilizofi-
chwa zilivyotafutwa!

7 Wamekufukuza hadi mpa-
kani.

4 *Au labda, "ukiruka juu."

1 *Maana yake "Mtumishi wa Yehova."

Washirika wako wote* wamekudanganya.

Watu walio na amani pamoja nawe wamekushinda.

Wale wanaokula mkate pamoja nawe wataweka wavu chini yako,

Lakini hutatambua.

8 Katika siku hiyo," asema Yehova,

"Je, sitawaangamiza wenye hekima kutoka Edomu^a

Na wenye utambuzi walio katika eneo lenye milima la Esau?

9 Na mashujaa wako wataogopa,^b Ee Temani,^c

Kwa kuwa kila mtu aliye katika eneo lenye milima la Esau atauawa kwa upanga.^d

10 Kwa sababu ya ukatili uliomtendea ndugu yako Yakobo,^e

Aibu itakufunika,^f Nawe utaangamia milele.^g

11 Siku uliyosimama kando, Siku ambayo wageni walichukua jeshi lake na kulipeleka utekwani,^h

Wageni walipoingia katika lango lake na kugawana Yerusalemu kwa kura,ⁱ Ulitenda kama wao.

12 Hupaswi kucheka siku ambayo ndugu yako anapatwa na maafa,^j

Hupaswi kushangilia siku ambayo watu wa Yuda wanaangamia,^k

Nawe hupaswi kujigamba sana siku wanayotabika.

a Yer 49:7

b Yer 49:22

c Mwa 36:10, 11
Eze 25:13
Amo 1:12

d Isa 34:5, 6

e Mwa 27:41, 42
Hes 20:20, 21
Zb 83:4-6
Zb 137:7
Yoe 3:19
Amo 1:11

f Yer 49:13

g Mal 1:3, 4

h 2Fa 24:10, 16
Yer 52:28

i Yoe 3:3

j Mik 4:11

k Omb 4:21

Safu ya 2

a Zek 1:15

b Zb 137:7
Eze 25:12

c Amo 1:11

d Yer 30:7

e Yer 9:25, 26
Yer 25:32
Yoe 3:12, 14
Mik 5:15

f Eze 35:15

g Yer 25:17
Yer 49:12

h Yoe 2:32

i Isa 4:3
Zek 8:3

j Isa 14:2
Amo 9:11, 12

13 Hupaswi kuingia katika lango la watu wangu siku wanayopatwa na msiba,^a Hupaswi kuwacheka siku wanayopatwa na msiba, Nawe hupaswi kuchukua mali yao siku wanayopatwa na msiba.^b

14 Hupaswi kusimama kwenye makutano ya barabara ili kuwachinja watu wake wanaokimbia,^c Nawe hupaswi kuwakabidhi waokokaji kwa maa-ndui wao siku wanayopatwa na taabu.^d

15 Kwa maana siku ya Yehova ya kuhukumu mataifa yote inakaribia.^e

Kama ulivyofanya, ndivyo utakavyofanyiwa.^f

Utatendewa kama ulivyo-watendea wengine.

16 Kwa maana kama mliyokunywa divai kwenye mlima wangu mtakatifu, Ndivyo mataifa yote yata-kavyoendelea kunywa hasira yangu kama divai.^g

Yatakunywa na kumeza hasira yangu,

Nayo yatatoweka kana kwamba hayajawahi kuwepo.

17 Lakini wale watakaookoka watakuwa juu ya Mlima Sayuni,^h

Nao utakuwa mtakatifu;ⁱ Na nyumba ya Yakobo itamiliki mali yao.^j

18 Nyumba ya Yakobo itakuwa moto, Nyumba ya Yosefu itakuwa mwali wa moto, Na nyumba ya Esau itakuwa kama majani makavu;

7 *Au "Wale wote waliofanya agano pamoja nawe."

Watayachoma moto na ku-
yateketeza,
Na hakuna atakayeokoka
katika nyumba ya Esau,^a
Kwa maana Yehova mwe-
nyewe amesema.

19 Watamiliki Negebu na
eneo lenye milima la
Esau,^b

Shefela na nchi ya Wafi-
listi.^c

Watamiliki shamba la
Efraimu na shamba la
Samaria,^d

Na Benjamini atamiliki
Gileadi.

a Yer 49:17, 18
Eze 35:15

b Amo 9:11, 12

c Isa 11:14
Amo 1:8

d 2Fa 17:24
Yer 31:5, 6

Safu ya 2

a Zb 122:6, 7

b 1Fa 17:9

c Yer 13:19
Yer 33:13

d Zb 149:6, 7
Eze 35:11

e Zb 22:28
Zek 14:9

20 Waliohamishwa kutoka ka-
tika boma hili, ^{*a}

Naam, Waisraeli, watami-
liki nchi ya Wakanaani
mpaka Sarefathi.^b

Na waliohamishwa kutoka
Yerusalemu, waliokuwa
Sefaradi, watamiliki ma-
jiji ya Negebu.^c

21 Na waokoaji watapanda
Mlima Sayuni

Ili kuhukumu eneo lenye
milima la Esau,^d

Na ufalme utakuwa wa Ye-
hova.”^e

20 *Au “ngome hii.”

YONA

YALIYOMO

- 1 Yona ajaribu kumkimbia Yehova (1-3)
Yehova aleta dhoruba kali (4-6)
Yona ndiye chanzo cha taabu (7-13)
Yona atupwa ndani ya bahari
iliyoachafuka (14-16)
Samaki mkubwa ammeza Yona (17)
- 2 Yona asali akiwa ndani ya tumbo la
samaki (1-9)
Yona atapikwa kwenye nchi kavu (10)
- 3 Yona amtii Mungu na kwenda
Ninawi (1-4)

Waninawi watubu baada ya kusikia
ujumbe wa Yona (5-9)
Mungu aamua kutoangamiza
Ninawi (10)

- 4 Yona akasirika, atamani kufa (1-3)
Yehova amfundisha Yona kuhusu
rehema (4-11)
“Je, una sababu nzuri ya kuwaka
hasira?” (4)
Somo la mmung’unye (6-10)

1 Neno hili la Yehova lilimjia
Yona^{*a} mwana wa Amitai:
2 “Inuka, nenda Ninawi^b lile
jiji kubwa, ukatangaze huku-
mu dhidi ya jiji hilo kwa saba-
bu nimeona uovu wao.”

3 Lakini Yona akainuka na
kwenda Tarshishi ili amki-
mbie Yehova; akashuka kwe-

1:1 *Maana yake “Njiwa.”

SURA YA 1

a 2Fa 14:25
Lu 11:29, 30

nda Yopa, akakuta meli inayo-
kwenda Tarshishi. Basi akali-
pa nauli na kupanda meli ili
asafiri nao kwenda Tarshishi,
amkimbie Yehova.

4 Ndipo Yehova akavumisha
upepo mkali baharini, dho-
ruba* kali sana ikatokea
baharini hivi kwamba meli

b Mt 12:41

1:4 *Au “tufani.”

ikawa karibu kuvunjika-vunjika. **5** Mabaharia wakao-gopa sana hivi kwamba kila mmoja wao akaanza kumlilia mungu wake amsaidie. Nao wakaanza kutupa baharini vitu vilivyokuwa melini ili kupunguza uzito wa meli.^a Lakini Yona alikuwa ameshuka chini ndani ya meli,* ambamo alikuwa amelala na kushikwa na usingizi mzito. **6** Nahodha wa meli akamkaribia na kumuuliza: “Kwa nini unalala? Amka, mwombe mungu wako! Huenda Mungu wa kweli ataturumia, nasi hatutaangamia.”^b

7 Ndipo mabaharia wakaa- mbiana: “Njooi, tupige kura^c ili tujue chanzo cha taabu hii.” Basi wakapiga kura, na kura zikamwangukia Yona.^d **8** Wakamuuliza: “Tafadhali tua- mbie, ni nani anayetusababi- shia taabu hii? Unafanya kazi gani, na unatoka wapi? Unatoka nchi gani, na wewe ni mtu wa kabila gani?”

9 Akawajibu: “Mimi ni Mwe- brania, nami namwogopa* Ye- hova Mungu wa mbinguni, Ali- yeumba bahari na nchi kavu.”

10 Waliposikia hayo, wa- naume hao wakazidi kuogo- pa, wakamuuliza: “Umefanya nini?” (Watu hao wakagundua kwamba alikuwa akimkimbia Yehova, kwa sababu Yona ali- waambia.) **11** Basi wakamu- uliza: “Tukufanye nini ili ba- hari itulie kwa ajili yetu?” Kwa sababu bahari ilizidi kuchafu- ka. **12** Akawajibu: “Nibebe- ni mnitupe baharini, na baha- ri itatulia kwa ajili yenu; kwa maana najua kwamba dhoru- ba hii kali imewapata kwa sa-

1:5 *Au “chombo chenye sitaha.” 1:9 *Au “namwabudu.”

SURA YA 1

a Mdo 27:18, 38

b Yon 3:9

c Met 16:33
Met 18:18d Yos 7:14, 18
1Sa 14:42, 43

Safu ya 2

a Da 6:26, 27

b Mt 12:39, 40
Mt 16:4
Lu 11:29, 30

SURA YA 2

c Zb 91:14, 15
Mt 12:40

d Zb 120:1

e Zb 130:1, 2

f Zb 69:1

g Zb 42:7

babu yangu.” **13** Hata hivyo, wanaume hao wakapiga ma- kasia kwa nguvu* ili kuirudi- sha meli kwenye nchi kavu, la- kini wakashindwa kwa sababu dhoruba ilizidi kuwa kali.

14 Kisha wakamlilia Yehova wakisema: “Jamani, sasa, Ee Yehova, tafadhali, tunakusihi usituangamize kwa sababu ya mtu huyu!* Usituadhibu kwa sababu ya damu isiyo na ha- tia, kwa kuwa umefanya upe- ndavyo, Ee Yehova!” **15** Basi wakambeba Yona na kumtu- pa baharini; na bahari ikatu- lia. **16** Kisha wanaume hao wakamwogopa sana Yehova,^a nao wakamtolea Yehova dha- bihu na kumwekea nadhiri.

17 Kisha Yehova akamtu- ma samaki mkubwa ammeze Yona, basi Yona akakaa ndani ya tumbo la samaki huyo kwa siku tatu, mchana na usiku.^b

2 Ndipo Yona akiwa ndani ya tumbo la samaki akasa- li kwa Yehova Mungu wake,^c **2** na kusema:

“Katika taabu yangu nili- mlilia Yehova, naye aka- nijibu.^d

Nikiwa ndani ya* Kaburi[#] nilililia msaada.^e

Uliisikia sauti yangu.

3 Uliponitupa katika vilindi, katikati ya* bahari, Ndipo mikondo ya maji ikanifunika.^f

Mawimbi yako yote maku- bwa na yale yanayoishia ufuoni yakanifunika.^g

4 Nami nikasema, ‘Nimefu-

1:13 *Au “wakajitahidi kutafuta njia.”

1:14 *Au “kwa sababu ya nafsi ya mtu huyu.” 2:2 *Tnn., “katika tumbo la.” #Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:3 *Tnn., “katika moyo wa.”

kuzwa kutoka mbele za macho yako!

Nitalikaziaje macho tena hekalu lako takatifu?

5 Maji yalinifunika na kuhtarisha uhai wangu;*^a

Kilindi cha maji kilinizunguka.

Kichwa changu kilisokotwa na magugu maji.

6 Nilizama sehemu za chini za milima.

Milango ya dunia ilikuwa ikija kunifungia milele.

Lakini uliutoa uhai wangu shimoni, Ee Yehova Mungu wangu.^b

7 Uhai wangu ulipokuwa ukitoka polepole, Yehova Ndiye niliyemkumbuka.^c

Ndipo sala yangu ikakufikia, ndani ya hekalu lako takatifu.^d

8 Wale wanaoabudu sanamu ambazo ni ubatili huacha chanzo chao cha upendo mshikamanifu.*

9 Lakini mimi, kwa sauti ya shukrani nitakutolea dhabihu.

Nadhiri nilizoweka, nitazitimiza.^e

Wokovu unatoka kwa Yehova."^f

10 Baadaye Yehova akamwamuru huyo samaki, naye akamtapika Yona kwenye nchi kavu.

3 Ndipo neno la Yehova likamjia Yona mara ya pili likisema:^g **2** "Inuka, nenda Ninawi^h lile jiji kubwa, ukalitangazie ujumbe ninaokuambia."

3 Basi Yona akatii neno la Yehova,ⁱ akainuka na kwenda Ninawi.^j Sasa Ninawi lilikuwa

2:5 * Au "Maji yaliizunguka nafsi yangu."
2:8 * Au labda, "cha ushikamanifu."

SURA YA 2

a Zb 69:1

b Zb 16:10
Zb 30:3
Isa 38:17
Mdo 2:31

c Zb 142:2, 3
Zb 143:4, 5

d Zb 18:6

e Zb 50:14

f Zb 3:8
Isa 12:2

SURA YA 3

g Yon 1:1, 2

h Mwa 10:8, 11
Nah 1:1
Sef 2:13

i Yon 2:9

j Mwa 10:8, 11

Safu ya 2

a Kut 9:20
Mt 12:41
Lu 11:32

b Lu 11:32

c Yer 18:7, 8
Eze 18:21-23
Yon 4:2

jiji kubwa sana*—mtu anayete-mbea kwa miguu angezunguka jiji hilo kwa siku tatu. **4** Ndipo Yona akaingia jijini, akate-mbea safari ya siku moja akitangaza hivi: "Bado siku 40 tu, jiji la Ninawi litaangamizwa."

5 Watu wa Ninawi wakamwamini Mungu,^a nao wakatangaza watu wafunge na kuvaa magunia, kuanzia aliye mkubwa zaidi hadi aliye mdogo zaidi. **6** Ujumbe huo ulipomfikia mfalme wa Ninawi, alinuka kutoka kwenye kiti chake cha ufalme, akavua vazi lake la kifalme, akavaa nguo za magunia, na kuketi katika majivu. **7** Pia, akaamuru tangazo hili litolewe katika jiji lote la Ninawi:

"Kwa agizo la mfalme na wakuu wake: Hakuna mwanadamu yeyote wala mnyama yeyote wa kufugwa anayepaswa kula kitu chochote. Hawapaswi kula chakula wala hawapaswi kunywa maji. **8** Wote wavae magunia, mwanadamu na mnyama; na wamwite Mungu kwa bidii na kuacha njia zao ovu na matendo yao ya ukatili. **9** Ni nani anayeuja ikiwa Mungu wa kweli hatafikiria upya* jambo analokusudia kufanya na kuacha hasira yake inayowaka, ili tusiangamie?"

10 Mungu wa kweli alipooa waliyofanya, jinsi waliyvoacha njia zao ovu,^b akafikiria upya kuhusu* msiba aliosema kwamba angewaletea, naye hakuuleta.^c

4 Lakini jambo hilo lilimchukiza sana Yona, akakasirika sana. **2** Basi akasali hivi

3:3 *Tnn., "jiji kubwa mbele za Mungu."
3:9 * Au "hataghairi kuhusu." 3:10 * Au "akaghairi kuhusu."

kwa Yehova: “Ee Yehova, je, sikujua utafanya jambo hili nilipokuwa katika nchi yangu? Ndiyo sababu tangu awali nilijaribu kukimbilia Tarshishi;^a kwa maana nilijua kwamba wewe ni Mungu mwenye huruma* na rehema, hukasiriki upesi, una upendo mwingi mshikamanifu,^b na unahuzunishwa na msiba. **3** Sasa, Ee Yehova, nakusihi unieue, kwa maana afadhali nife badala ya kuishi.”^c

4 Yehova akamuuliza: “Je, una sababu nzuri ya kuwaka hasira?”

5 Ndipo Yona akatoka jijini, akaketi chini upande wa mashariki wa jijii. Akajenga kibanda hapo na kuketi kivulini ili aone jambo litakalolipata jijii hilo.^d **6** Kisha Yehova Mungu akaotesha mmung’unye* ili Yona apate kivuli kwa ajili ya kichwa chake na ili kupunguza taabu yake. Basi Yona akaufurahia sana mmung’unye huo.

7 Lakini siku iliyofuata, wakati wa mapambazuko, Mungu

4:2 *Au “neema.” **4:6** *Au labda, “mbarika; mnyoyo; mbono.”

SURA YA 4

a Yon 1:3

b Kut 34:6

Zb 78:38

Zb 86:5

Zb 145:8

c Hes 11:11,15

1Fa 19:2,4

Ayu 6:8,9

d Yon 3:4

Safu ya 2

a Yon 4:3

b Yon 4:4

c Yon 3:3

d Zb 36:6

Zb 145:9

wa kweli akamwamuru kiwavi aushambulie mmung’unye huo, nao ukanyauka. **8** Joto la jua lilipoanza kuongezeka, Mungu akaleta pia upepo wa mashariki wenye joto kali, na jua likamchoma Yona kichwani, karibu azimie. Akaendelea kuomba afe,* na kuendelea kusema: “Afadhali nife badala ya kuishi.”^a

9 Mungu akamuuliza Yona: “Je, una sababu nzuri ya kuwaka hasira kwa sababu ya mmung’unye?”^b

Ndipo Yona akasema: “Nina sababu nzuri ya kukasirika, nimekasirika sana hivi kwamba natamani kufa.” **10** Lakini Yehova akamwambia: “Uliuhurumia mmung’unye ambao hukuufanya kazi yoyote wala kuukuza; uliota na kukua usiku mmoja na kunyauka usiku uliofuata. **11** Je, mimi pia sipaswi kulihurumia jijii kubwa la Ninawi,^c ambalo lina watu zaidi ya 120,000 ambao hata hawajui kutofautisha jema na baya,* na kuwahurumia pia wanyama wao wengi?”^d

4:8 *Au “kuomba nafsi yake ife.” **4:11** *Au “tofauti kati ya mkono wao wa kulia na wa kushoto.”

MIKA

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Hukumu dhidi ya Samaria na Yuda (1-16)
Matatizo yasababishwa na dhambi na uasi (5)</p> <p>2 Ole kwa wakandamizaji! (1-11)
Waisraeli wakusanywa na kuunganishwa (12, 13)
Nchi itakuwa na kelele za watu (12)</p> | <p>3 Viongozi na manabii washutumiwa (1-12)
Mika apata nguvu nyingi kwa sababu ya roho ya Yehova (8)
Makuhani wafundisha ili wapate pesa (11)
Yerusalemu litabaki marundo ya magofu (12)</p> |
|--|--|

- 4 Mlima wa Yehova wainuliwa (1-5)
Panga zitakuwa majembe (3)
"Tutatembea katika jina la Yehova" (5)
Sayuni lajengwa upya na kuimarishwa (6-13)
- 5 Mtawala atakayekuwa mkuu katika dunia yote (1-6)
Mtawala atatoka Bethlehemu (2)
Watu waliobaki watakuwa kama umande na kama simba (7-9)
Nchi itatakaswa (10-15)
- 6 Mungu ana kesi dhidi ya Waisraeli (1-5)
Yehova anataka nini? (6-8)
Haki, ushikamanifu, kiasi (8)
Hatia na adhabu ya Waisraeli (9-16)
- 7 Maadili mapotovu ya Waisraeli (1-6)
Adui watakuwa watu wa nyumbani (6)
"Nitaonyesha mtazamo wa kumngojea Mungu" (7)
Watu wa Mungu watetewa (8-13)
Mika asali na kumsifu Mungu (14-20)
Jibu la Yehova (15-17)
'Ni Mungu gani aliye kama Yehova?' (18)

1 Neno la Yehova lililomjia Mika^a wa Moreshethi, katika siku za utawala wa Yothamu,^b Ahazi,^c na Hezekia,^d wafalme wa Yuda,^e na ambalo alilipokea katika maono kuhusu Samaria na Yerusalemu:

- 2** "Sikieni, enyi mataifa yote!
Sikiliza, Ee dunia na vitu vyote vinavyokujaza,
Acha Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova awe shahidi dhidi yako^f
—Yehova kutoka katika hekalu lake takatifu.
- 3** Kwa maana tazama! Yehova anatoka mahali pake; Atashuka chini na kukanyaga sehemu za juu za dunia.
- 4** Milima itayeyuka chini yake,^g
Na mabonde yatagawanyika*
Kama nta mbele ya moto,

1:1 *Ufupisho wa jina Mikaeli (linaloamaanisha "Ni Nani Aliye Kama Yehova?") au Mikaya (linaloamaanisha "Ni Nani Aliye Kama Yehova?"). 1:4 *Au "nchi tamarare za chini zitagawanyika."

SURA YA 1

a Yer 26:18

b 2Fa 15:32-34
2Nya 27:1, 2

c 2Fa 16:1, 2

d 2Fa 18:1-3
2Nya 29:1, 2e Isa 1:1
Ho 1:1

f Zb 50:7

g Amu 5:5
Zb 97:5

Safu ya 2

a 2Fa 17:7, 8

b Ho 7:1

c 2Fa 16:2, 4

d Law 26:30
Ho 8:6e Ho 2:5
Ho 9:1

Kama maji yanayomwagwa kwenye mteremko mkali.

- 5** Hayo yote kwa sababu ya uasi wa Yakobo, Kwa sababu ya dhambi za nyumba ya Israeli.^a
Uasi wa Yakobo ni nini? Je, si Samaria?^b
Na mahali pa juu pa Yuda ni nini?^c
Je, si Yerusalemu?
- 6** Nitafanya Samaria kuwa rundo la magofu la shambani,
Mahali pa kupanda mizabibu;
Nitayatupa* mawe yake chini bondeni,
Nami nitaichimbua misingi yake.
- 7** Sanamu zake zote za kuchongwa zitavunjwa vipandevipande,^d
Na zawadi zote alizopewa kwa sababu ya ukahaba wake zitateketezwa motoni.^e
Nitaharibu kabisa sanamu zake zote.

1:6 *Tnn., "Nitayamwaga." 1:7 *Au "malipo yote ya ukahaba wake yatateketezwa motoni."

Kwa sababu alizikusanya
kwa kutumia malipo ya
ukahaba,
Nazo zitakuwa tena malipo
ya makahaba.”

- 8** Kwa sababu hiyo nitalia
kwa sauti na kupiga ma-
yowe;^a
Nitatembea bila viatu niki-
wa uchi.^b
Nitalia kwa sauti kama
mbwamwitu wanavyolia,
Na kuomboleza kama mbu-
ni wanavyoomboteza.
- 9** Kwa sababu jeraha lake
haliwezi kuponywa;^c
Limefika mpaka Yuda.^d
Pigo limeenea mpaka kwe-
nye lango la watu wangu,
mpaka Yerusalemu.^e
- 10** “Msitangaze hilo kule Ga-
thi;
Msilie hata kidogo.
Kule Beth-afra* mgaegae
mavumbini.
- 11** Vukeni mkiwa uchi na we-
nye aibu, enyi wakaaji*
wa Shafiri.
Wakaaji wa Saanani hawa-
jatoka nje.
Kutakuwa na kilio kikubwa
kule Beth-ezeli, nacho
hakitawasaidia.
- 12** Kwa maana wakaaji wa
Marothi wamengojea
mema,
Lakini mabaya yameshuka
kutoka kwa Yehova mpa-
ka kwenye lango la Yeru-
salemu.
- 13** Fungeni kundi la farasi
kwenye gari la vita, enyi
wakaaji wa Lakishi.^f
Mlikuwa chanzo cha dha-
mbi kwa binti ya Sayuni,
Kwa maana maasi ya

1:10 *Au “Katika nyumba ya Afra.” 1:11
*Tnn., “ewe mkaaji wa kike.”

SURA YA 1

a Yer 4:19

b Isa 20:2

c Isa 1:5, 6
Yer 15:18

d 2Fa 18:13
Isa 8:7, 8

e 2Nya 32:2
Mik 1:12

f Yos 15:20, 39
2Fa 18:14

Safu ya 2

a 1Fa 14:16
2Fa 16:2, 3
Yer 3:8

b Yos 15:20, 44

c Isa 7:17

d 2Nya 11:5, 8

e Ne 11:25, 30

f Kum 28:41
2Fa 17:6
Isa 39:7

SURA YA 2

g 1Fa 21:7

h Kut 20:17
1Fa 21:2
Isa 5:8

i Yer 22:17
Eze 22:12, 29

j Yer 18:11

k Amo 2:14

Israeli yalipatikana nda-
ni yako.^a

- 14** Kwa hiyo mtampa
Moresheth-gathi za-
wadi za kumuaga.*
Nyumba za Akzibu^b ziliku-
wa kitu cha udanganyifu
kwa wafalme wa Israeli.
- 15** Bado nitawaletoa
mshindi,^{*c} enyi wakaaji
wa Maresha.^d
Utukufu wa Israeli utafika
mpaka Adulamu.^e
- 16** Nyoeni upara na kuzikata
kabisa nywele zenu kwa
ajili ya watoto wenu wa-
pendwa.
Nyoeni upara kama wa tai,
Kwa maana wamechuku-
liwa kutoka kwenu na
kupelekwa uhamishoni.”^f
- 2** “Ole wao wanaopanga nja-
ma yenye kudhuru,
Wanaotunga maovu vita-
ndani mwao!
Kunapambazuka wana-
yatekeleza,
Kwa sababu wana uwezo
wa kuyatekeleza.^g
- 2** Wanatamani mashamba
na kuyanyakua;^h
Pia nyumba, na kuzi-
chukua;
Wanamlaghai mtu na ku-
chukua nyumba yake,ⁱ
Wanachukua urithi
wa mtu.
- 3** Kwa hiyo Yehova anasema
hivi:
‘Sasa basi nakusudia kui-
letea familia hii msiba^j
ambao hamtaweza kuue-
puka.*^k
Hamtatembea tena kwa

1:14 *Au “za kwaheri.” 1:15 *Au
“mnyang’anyi.” 2:3 *Tnn., “hamtauo-
ndoa kwenye shingo zenu.”

kiburi,^a kwa sababu utakuwa wakati wa msiba.^b

- 4 Siku hiyo watu watatunga methali kuwahusu, Nao watawaombolezea kwa uchungu.^c

Watasema: “Tumeangamizwa kabisa!^d

Alisababisha fungu la watu wangu lichukuliwe na wengine—Lo! Ameni-pokonya!^e

Amemgawia yule asiye mwaaminifu mashamba yetu.”

- 5 Kwa hiyo hamtakuwa na mtu wa kunyoosha kamba ya kupimia, Wa kuigawa ardhi katika kutaniko la Yehova.

- 6 Wanahubiri wakisema, “Acheni kuhubiri!”

“Hawapaswi kuhubiri mambo haya; Hatutapatwa na aibu!”

- 7 Je, inasemwa, Ee nyumba ya Yakobo, kwamba “Roho ya Yehova imekosa subira?

Je, haya ndiyo matendo yake?”

Je, maneno yangu mwenyewe hayawanufaishi wale wanaotembea kwa unyoofu?

- 8 Lakini hivi karibuni watu wangu mwenyewe wameinuka kama adui.

Mnalivua hadharani pamba la kifahari pamoja na* vazi

Kutoka kwa watu wanaopita bila wasiwasi, kama watu wanaorudi kutoka vitani.

- 9 Mnawafukuza wanawake wa watu wangu kutoka

SURA YA 2

a Isa 2:11

b Amo 5:13

c Yer 9:10
Omb 1:1

d Isa 6:11
Yer 25:9
Sef 1:2

e 2Fa 17:23

Safu ya 2

a Zb 106:38, 39

b Yer 9:19
Yer 10:18

c 1Fa 22:6, 8
Isa 9:15, 16
Yer 6:13, 14
Eze 13:2, 3

d Isa 11:11
Yer 23:3
Yer 31:7, 8
Mik 4:6

e Eze 34:11

f Eze 36:38
Zek 8:22

g Isa 62:10

h Isa 49:10
Isa 52:12

SURA YA 3

i Mik 3:9

katika nyumba zao zenye kupendeza;

Mnaondoa fahari yangu milele kutoka kwa watoto wao.

- 10 Inukeni mwende zenu, kwa sababu hapa si mahali pa kupumzika.

Kwa sababu ya uchafu,^a kuna maangamizi, maangamizi makubwa.^b

- 11 Mtu akifuata upepo na udanganyifu na kusema uwongo huu:

“Nitawahubiria kuhusu divai na pombe,”

Basi atakuwa mhubiri anayewafaa kabisa watu hawa!^c

- 12 Kwa hakika nitawakusanya ninyi nyote, enyi watu wa Yakobo;

Kwa kweli nitawakusanya pamoja wale wanaobaki wa Israeli.^d

Kwa umoja nitawaweka kama kondoo zizini,

Kama kundi la kondoo katika malisho yake;^e

Litakuwa na kelele za watu.^f

- 13 Yule anayevunja lango na kutoka atawatangulia;

Nao watavunja lango na kupitia langoni kwenenda nje.^g

Mfalme wao atapitia humo akiwatangulia,

Huku Yehova akiwangoza.^h

- 3 Nilisema: “Sikieni, tafadhali, enyi viongozi wa Yakobo

Nanyi makamanda wa nyumba ya Israeli.ⁱ

Je, hampaswi kujua jambo lililo la haki?

2:8 * Au labda, “kutoka kwenye.”

- 2** Lakini mnachukia mema^a na kupenda maovu;^b Mnawachuna ngozi watu wangu na kuondoa nyama kutoka kwenye mifupa yao.^c
- 3** Pia mnakula nyama ya watu wangu^d Na kuwachuna ngozi, Mnapasua mifupa yao, na kuivunja vipande-vipande,^e Kama kitu kinachopikwa ndani ya chungu,^{*} kama nyama ndani ya chungu cha kupikia.
- 4** Wakati huo watamlilia Yehova awasaidie, Lakini hatawajibu. Atauficha uso wake kutoa kwao wakati huo,^f Kwa sababu ya matendo yao maovu.^g
- 5** Yehova anasema hivi kuhusu manabii wanaowapotosha watu wake,^h Wanaotangaza 'Amani!'ⁱ huku wakitafuna^{*} kwa meno yao^j Lakini wanaotangaza[#] vita dhidi ya yule asiyeweka kitu vinywani mwao:
- 6** 'Mtakuwa na usiku,^k haku-takuwa na maono;^l Mtakuwa na giza tu, haku-takuwa na uaguzi.^{*} Jua litatua kwa manabii, Na mchana utageuka kuwa giza kwao.^m
- 7** Watu wanaoona maono wataaibishwa,ⁿ

3:3 *Au "chungu cha kupikia chenye mdomo mpana." 3:5 *Au labda, "wanapokuwa na kitu cha kutafuna." #Tnn., "wanaotakasa." 3:6 *Au "ubashiri."

SURA YA 3

- a 1Fa 22:8
Amo 5:10
- b 2Nya 19:2
- c Eze 22:27
Amo 8:4
Sef 3:3
- d Eze 34:2, 3
- e Isa 3:15
- f Omb 3:44
- g Kum 31:17, 18
Isa 1:15
Isa 3:11
- h Isa 9:15, 16
Isa 56:10
- i Yer 23:16, 17
Eze 13:10
- j Eze 13:19
Eze 34:2
- k Yer 13:16
- l Zb 74:9
Eze 13:23
- m Isa 59:9, 10
Amo 8:9
- n Isa 29:10

Safu ya 2

- a Mik 3:1
- b Kum 27:19
Yer 5:28
- c Yer 22:13
- d Isa 1:23
Isa 5:20, 23
Eze 22:12
- e Yer 6:13
- f Isa 56:10, 11

g Isa 48:1, 2
Yer 7:4

h Amo 9:10

- Na wabashiri watakata tamaa.
Wote watalazimika kufunika masharubu,^{*} Kwa maana hakuna jibu kutoka kwa Mungu."[†]
- 8** Lakini mimi, nimejazwa nguvu kwa roho ya Yehova,
Nimejazwa haki na uwezo,
Ili nimwambie Yakobo uasi wake na Israeli dhambi yake.
- 9** Sikieni jambo hili, tafadhali, enyi viongozi wa nyumba ya Yakobo Nanyi makamanda wa nyumba ya Israeli,^a Mnaochukia haki na kupotosha mambo yote yali-yonyooka,^b
- 10** Mnaojenga Sayuni kwa umwagaji wa damu na Yerusalemu kwa ukosefu wa uadilifu.^c
- 11** Viongozi^{*} wake huhukumu ili wapate rushwa,^d Makuhani wake hufundisha ili wapate malipo,^e Na manabii wake hufanya uaguzi[#] ili wapate pesa.^{△f} Na bado wanamwegemea Yehova,^g wakisema: "Je, Yehova hayuko pamoja nasi?^g Hakuna msiba utakaotupata."^h
- 12** Basi kwa sababu yenu, Sayuni litalimwa kama shamba,

3:7 *Au "watafumba vinywa vyao." 3:11 *Tnn., "Vichwa." #Au "hubashiri." △Au "fedha." gAu "wanadai wanamwegemea Yehova."

Yerusalemu litakuwa marundo ya magofu,^a
Na mlima wa Nyumba* utakuwa kama vilima msituni.^{#b}

- 4** Katika siku za mwisho,* Mlima wa nyumba ya Yehova^c
Utaimarishwa kabisa juu ya vilele vya milima,
Nao utainuliwa juu ya vilima,
Na mataifa yatamiminika kwenye mlima huo.^d
- 2** Na mataifa mengi yataenda na kusema:
“Njooi, twendeni juu kwenye mlima wa Yehova
Na kwenye nyumba wa Mungu wa Yakobo.^e
Naye atatufundisha njia zake,
Nasi tutatembea katika vijia vyake.”
Kwa maana sheria itatoka* Sayuni,
Na neno la Yehova litatoka Yerusalemu.
- 3** Atatekeleza hukumu miongoni mwa mataifa mengi^f
Na kunyoosha* mambo kuhusiana na mataifa yenye nguvu yaliyo mbali.
Watafua panga zao ziwe majembe ya plau
Na mikuki yao iwe miundu.^g
Taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine,
Wala hawatajifunza vita tena kamwe.^h

3:12 *Au “mlima wa hekalu.” #Au “kili-
ma chenye msitu.” 4:1 *Au “Katika ki-
pindi cha mwisho cha zile siku.” 4:2
*Au “mafundisho yatatoka.” 4:3 *Au
“kurekebisha.”

SURA YA 3

a Zb 79:1

b Yer 26:18

SURA YA 4

c Isa 11:9

Zek 8:3

d Zb 86:9

Isa 2:2-4

Isa 60:3

Ufu 15:4

e Yer 31:6

Zek 8:20, 21

f Isa 2:10

Zb 96:13

Isa 51:4, 5

g Ho 2:18

Zek 9:10

h Zb 72:7

Isa 9:7

Isa 60:18

Safu ya 2

a Zek 3:10

b Isa 54:14

Eze 34:25

Eze 39:25, 26

c Zek 10:12

d Zb 147:2

Isa 56:8

Eze 34:12, 16

Eze 37:21

Sef 3:19

e Isa 10:21

Mik 2:12

Mik 7:18

f Isa 60:22

g 2Sa 5:7

h Oba 21

i Zek 9:9

- 4** Wataketi,* kila mtu chini ya mzabibu wake na chini ya mtini wake,^a
Na hakuna yeyote atakaye-
waogopesha,^b
Kwa maana kinywa cha Yehova wa majeshi kimesema hoya.
- 5** Kwa maana mataifa yote yatatembea, kila taifa katika jina la mungu wake,
Lakini sisi tutatembea katika jina la Yehova Mungu wetu^c milele na milele.
- 6** “Siku hiyo,” asema Yehova,
“Nitamkusanya yule aliye-
kuwa akichechemea,
Na kumkusanya pamoja yule aliyetawanyika,^d
Pamoja na wale niliowatesa.
- 7** Nitamfanya yule aliyeku-
wa akichechemea abaki,^e
Na yule aliyepelekwa mbali kuwa taifa lenye nguvu;^f
Na Yehova atawatawala akiwa mfalme katika Mlima Sayuni,
Kuanzia sasa mpaka milele.
- 8** Lakini wewe, Ee mnara wa kundi,
Kilima cha binti ya Sayuni,^g
Kwako wewe utakuja, naam, utawala wa kwanza* utakuja,^h
Ufalme ambao ni wa binti ya Yerusalemu.ⁱ
- 9** Sasa kwa nini unapiga kelele?
Je, huna mfalme,

4:4 *Au “Wataishi.” 4:8 *Au “awali.”

- Au je, mshauri wako amean-gamia,
Hivi kwamba umeshikwa
na uchungu kama mwanamke anayezaa?^a
- 10** Gaagaa na kulia kwa uchungu, Ee binti ya Sayuni,
Kama mwanamke anayezaa,
Kwa maana sasa utatoka jijini na kuishi shambani.
Utaenda mpaka Babiloni,^b
Na huko utaokolewa;^c
Huko Yehova atakununua tena kutoka mikononi mwa maadui wako.^d
- 11** Sasa mataifa mengi yatakusanyika dhidi yako;
Yatasema, 'Acheni achafu-liwe,
Macho yetu na yaone Sayuni likipatwa na jambo hili.'
- 12** Lakini hawajui mawazo ya Yehova,
Hawaelewi kusudi* lake;
Kwa maana atawakusanya kwenye uwanja wa kupuria kama safu ya migan-da ya nafaka iliyotoka kukatwa.
- 13** Inuka upure, Ee binti ya Sayuni;^e
Kwa sababu nitabadili pe-mbe zako ziwe chuma,
Nami nitabadili kwato zako ziwe shaba,
Nawe utapondaponda ka-bisa mataifa mengi.^f
Faida yao isiyo ya haki utamtotea Yehova,
Na mali zao utampa Bwana wa kweli wa dunia yote."^g

SURA YA 4

- a Yer 30:6
- b 2Fa 20:18
2Nya 36:17, 20
- c Zb 107:2, 3
Isa 48:20
Yer 15:21
- d Isa 45:13
Zek 2:7
- e Isa 41:15
- f Zek 9:13
- g Yos 6:18, 19
Isa 23:17, 18
- Safu ya 2
- SURA YA 5
- a Kum 28:52
- b Mt 26:67
Yoh 18:22
Yoh 19:3
- c Mwia 35:19
Lu 2:4
- d Mwia 49:10
1Nya 5:2
Isa 9:6
Mt 2:4-6
Lu 1:32, 33
Lu 2:11
Yoh 7:42
- e Eze 34:23
Eze 37:24
- f Yer 23:5, 6
- g Zek 9:9, 10
- h Isa 9:6
- i Isa 8:7

- 5** "Sasa unajikatakata,
Ee binti unayeshambu-liwa;
Tumezingirwa.^a
Wanampiga mwamuzi wa Israeli shavuni kwa fimbo.^b
- 2** Na wewe, Ee Bethlehemu Efratha,^c
Uliye mdogo sana usiweze kuwa miongoni mwa maelfu ya * Yuda,^d
Kutoka kwako atatoka kwa ajili yangu yule atakaye-kuwa mtawala katika Israeli,
Ambaye asili yake ni ya tangu nyakati za kale, tangu siku za zamani za kale.
- 3** Kwa hiyo atawaacha Mpaka wakati ambapo mwanamke anayepaswa kuzaa atakapozaa.
Na wale ndugu zake wengine watarudi kwa watu wa Israeli.
- 4** Atasimama na kuchungu katika nguvu za Yehova,^e
Katika ukuu wa jina la Yehova Mungu wake.
Nao watakaa kwa usalama,^f
Kwa maana sasa ukuu wake utafika kwenye miisho ya dunia.^g
- 5** Naye ataleta amani.^h
Mwashuru akiivamia nchi yetu na kukanyaga-kanyaga minara yetu yenye ngome,ⁱ
Tutawainua wachungaji saba dhidi yake, naam, wakuu* wanane wana-damu.

4:12 *Au "shauri."

5:2 *Au "koo za." 5:5 *Au "viongozi."

- 6** Wataichunga nchi ya Ashuru kwa upanga,^a Na nchi ya Nimrodi^b kwenye malango yake. Naye atatuokoa kutoka kwa Mwashuru,^c Anapoivamia nchi yetu na kulikanyaga-kanyaga eneo letu.
- 7** Waliobaki wa Yakobo watakuwa miongoni mwa mataifa mengi Kama umande kutoka kwa Yehova, Kama manyunyu ya mvua juu ya mimea Ambayo hayatumaini mwanadamu Wala kuwangojea wana wa wanadamu.
- 8** Waliobaki wa Yakobo watakuwa miongoni mwa mataifa, Miongoni mwa mataifa mengi, Kama simba miongoni mwa wanyama wa mwituni, Kama mwanasimba* miongoni mwa makundi ya kondoo, Ambaye hupita na kurukia na kurarua vipandevipande; Wala hakuna yeyote wa kuwaokoa.
- 9** Mkono wako utainuliwa juu ya maadui wako, Na maadui wako wote wataangamizwa.”
- 10** “Siku hiyo,” asema Yehova, “Nitawaangamiza kabisa farasi wako na kuharibu magari yako ya vita.

5:8 * Au “mwanasimba mwenye manyoya marefu shingoni.”

SURA YA 5

a Isa 33:1

b Mwa 10:9-11

c Isa 14:25

Safu ya 2

a Isa 2:6
Isa 8:19b Isa 2:8
Eze 36:25
Ho 14:3
Zek 13:2

c Isa 27:9

SURA YA 6

d Isa 5:3

e Zb 50:1,4
Isa 1:2f Isa 43:26
Yer 2:35
Ho 4:1

g Yer 2:5

h Kut 12:51
Kum 4:20

i Kum 7:8

j Kut 15:20

- 11** Nitaharibu majiji yaliyo katika nchi yako Na kubomoa ngome zako zote.
- 12** Nitakomesha ulozi wako,* Na hakuna mchawi yeyote atakayebaki miongoni mwako.^a
- 13** Nitaharibu sanamu zako za kuchongwa na nguzo zako, Nawe hutainamia tena kazi ya mikono yako.^b
- 14** Nitang’oa miti yako mitakatifu*^c Na kuharibu kabisa majiji yako.
- 15** Kwa hasira na ghadhabu nitalipiza kisasi Dhidi ya mataifa ambayo hayajatii.”
- 6** Sikieni, tafadhali, jambo analosema Yehova. Simameni, pelekeni kesi mbele ya milima, Vilima na visikie sauti yenu.^d
- 2** Sikieni kesi ya Yehova, enyi milima, Enyi misingi imara ya dunia,^e Kwa maana Yehova ana kesi dhidi ya watu wake; Atateta dhidi ya Israeli:^f
- 3** “Watu wangu, nimewafanya nini? Nimewachoshaje?^g Toeni ushahidi dhidi yangu.
- 4** Kwa maana niliwapandisha kutoka nchini Misri,^h Kutoka katika nyumba ya utumwa niliwakomboa;ⁱ Nilimtuma Musa, Haruni, na Miriamu mbele yenu.^j

5:12 *Tnn., “kutoka mkononi mwako.”

5:14 * Angalia Kamusi, uku. 2012.

- 5** Watu wangu, tafadhali, kumbukeni pendekezo la Mfalme Balaki wa Moabu,^a
Na jibu ambalo Balaamu mwana wa Beori alimpa^b
—Kile kilichotukia kuanzia Shitimu^c mpaka Gilgali^d—
Ili mjue matendo ya uadilifu ya Yehova.”
- 6** Nitakuja mbele za Yehova nikiwa na nini?
Nitainama mbele za Mungu aliye juu nikiwa na nini?
Je, nitakuja mbele zake nikiwa na dhabihu nzima za kuteketezwa,
Nikiwa na ndama wenye umri wa mwaka mmoja?^e
- 7** Je, Yehova atapendezwa na maelfu ya kondoo dume,
Na makumi ya maelfu ya mito ya mafuta?^f
Je, nitamtoa mwanangu mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya uasi wangu,
Uzao wa mwili wangu kwa ajili ya dhambi yangu?^g
- 8** Ee mwanadamu, amekumbia yaliyo mema.
Na Yehova anataka * nini kutoka kwako?
Anataka tu utekeleze haki,^h uthamini sana ushikamanifu,ⁱ
Na utembe kwa kiasi^j na Mungu wako!^k
- 9** Sauti ya Yehova inaliita jiji;

6:7 *Au “dhambi ya nafsi yangu?” **6:8** *Au “anadai.” #Au “uwe mwenye haki; bila upendeleo.” ^Au “uwe mwenye fadhili na mshikamanifu katika upendo wako.” Tnn., “upende upendo mshikamanifu.”

SURA YA 6

a Hes 22:5, 6

b Hes 23:7, 8
Hes 24:10
Ufu 2:14c Hes 25:1
Hes 33:48, 49

d Yos 4:19

e 1Sa 15:22
Zb 51:16, 17
Isa 1:11

f Zb 50:8-15

g 2Fa 3:26, 27
Eze 16:20h Met 21:3
Isa 1:17
Yer 22:3
Eze 45:9
Ho 12:6i Met 3:3
Ho 6:6
Zek 7:9

j Met 8:13

k Kum 10:12, 13

Safu ya 2

a Isa 9:13

b Kum 25:13
Met 11:1
Ho 12:7c Isa 59:3
Mik 7:2

d Yer 9:3

e Isa 1:5

f Law 26:26
Eze 4:16
Ho 4:10g Kum 28:38
Yer 12:13
Yoe 1:10
Amo 5:11

Wale walio na hekima inayotumika wataliogopa jina lako.

Isikilizeni fimbo na yule aliyeichagua.^a

- 10** Je, bado kuna hazina za uovu katika nyumba ya mwovu

Na kipimo kilichopunguka cha efa* kinachochukiza?

- 11** Je, ninaweza kuwa safi ki-maadili* nikiwa na mizani ya uovu,

Nikiwa na mfuko wenye mawe ya kupimia ya udanganyifu?^b

- 12** Kwa maana matajiri wake wamejaa ukatili,

Na wakaaji wake husema uwongo;^c

Ulimi wao ni mdanganyifu kinywani mwao.^d

- 13** “Kwa hiyo, nitakupiga na kukujeruhi,^e

Na kukuacha katika hali ya ukiwa kwa sababu ya dhambi zako.

- 14** Utakula lakini hutashiba; Utahisi njaa.^f

Vitu utakavyotoa, hutaina navyo kwa usalama,

Na utakavyoenda navyo, nitaviharibu kwa upanga.

- 15** Utapanda mbegu, lakini hutavuna.

Utakanyaga-kanyaga zeituni, lakini hutatumia mafuta yake;

Nawe utatengeneza divai mpya, lakini hutakunywa divai hata kidogo.^g

- 16** Kwa maana unashika sheria za Omri na

6:10 *Angalia Nyongeza B14. **6:11** *Au “bila hatia.”

matendo yote ya nyumba ya Ahabu,^a

Nawe unafuata ushauri wao.

Ndiyo sababu nitakufanya kuwa kitu cha kutisha

Na wakaaji wake kuwa kitu cha kupigiwa mluzi;^b

Nawe utabeba dharau za mataifa.”^c

7 Ole wangu! Mimi ni kama mtu ambaye,

Baada ya matunda ya kiangazi kukusanywa

Na masalio kuokotwa baada ya mavuno ya zabibu,

Hapati kishada chochote cha zabibu za kula,

Wala tini inayoiva mapema ninayotamani kula.*

2 Mtu mshikamanifu ameanngamia* duniani;

Miongoni mwa wanadamu hakuna yeyote aliyemnyoofu.^d

Wote huvizia ili wamwage damu.^e

Kila mmoja anamwinda ndugu yake mwenyewe kwa wavu wa kukotwa.

3 Mikono yao ni stadi kati-ka kutenda maovu;^f

Mkuu anadai vitu, Hakimu anaomba zawadi,^g

Mtu maarufu anasema vitu anavyotamani,^{*h}

Nao hupanga njama pamoja.[#]

4 Aliye bora zaidi kati yao ni kama miiba,

SURA YA 6

a 1Fa 16:25, 30
2Fa 16:2, 3
2Fa 21:1, 3

b Yer 19:8

c Zb 44:13
Yer 51:51
Omb 5:1
Da 9:16

SURA YA 7

d Isa 57:1

e Isa 59:7

f Yer 3:5
Yer 4:22
Eze 22:6

g Isa 1:23
Mik 3:11

h 1Fa 21:5, 6

Safu ya 2

a Isa 10:3
Eze 12:23
Ho 9:7

b Isa 22:5

c Yer 9:4

d Eze 22:7

e Lu 12:53

f Yer 12:6
Mt 10:35, 36

g Zb 123:2
Isa 8:17

h Zb 25:5
Zb 62:1
Omb 3:26

i Zb 40:1
Isa 12:2
Isa 25:9

j Omb 1:18

Na mnyoofu zaidi kati yao ni mbaya zaidi kuliko uzio wa miiba.

Siku ya walenzi wako na siku utakayowajibishwa itakuja.^a

Sasa watashikwa na wasi-wasi.^b

5 Usimwamini mwenzako Wala usimtumaini rafiki wa karibu.^c

Uwe mwangalifu kuhusu mambo unayomwambia yule unayelala ukiwa umemkumbatia.

6 Kwa maana mwana anamdharau baba yake, Binti anashindana na mama yake,^d

Na binti mkwe anampinga mama mkwe wake;^e

Maadui wa mtu ni watu wa nyumbani mwake.^f

7 Lakini mimi, nitaendelea kumtazamia Yehova.^g

Nitaonyesha mtazamo wa kumngojea* Mungu wa wokovu wangu.^h

Mungu wangu atanisikia.ⁱ

8 Usishangilie juu yangu, ewe adui yangu.*

Ingawa nimeanguka, nita-simama;

Ingawa ninakaa gizani, Yehova atakuwa nuru yangu.

9 Ghadhabu ya Yehova nitavumilia

—Kwa maana nimemte-ndea dhambi—^j

Mpaka atakapoitetea kesi yangu na kutekeleza haki kwa ajili yangu.

7:1 *Au "ambayo nafsi yangu inatamani." 7:2 *Au "ametoweka." 7:3 *Au "tamaa ya nafsi yake." #Tnn., "huisko-kota pamoja."

7:7 *Au "Nitamngojea kwa subira." 7:8

*Katika Kiebrania, neno "adui" liko kati-ka jinsia ya kike.

Atanileta nje kwenye
nuru;
Nitautazama uadilifu
wake.

- 10** Adui yangu pia ataona,
Na aibu itamfunika yule
aliyeniambia:
“Yuko wapi Yehova Mungu
wako?”^a

Macho yangu yatamtaza-
ma adui yangu.
Sasa atakanyagwa-
kanyagwa kama
matope barabarani.

- 11** Itakuwa siku ya kujenga
kuta zako za mawe;
Siku hiyo mipaka itapa-
nuliwa.*
- 12** Siku hiyo watakuja
kwako

Watatoka mbali kule Ashu-
ru na katika majiji ya
Misri,
Kutoka Misri hadi kufika
Mto Efrati;
Kutoka bahari mpaka ba-
hari na kutoka mlima
mpaka mlima.^b

- 13** Na nchi itakuwa katika
hali ya ukiwa kwa saba-
bu ya wakaaji wake,
Kwa sababu ya mambo
waliyotenda.*

- 14** Wachunge watu wako kwa
famungu yako, kundi la uri-
thi wako,^c

Yule aliyekuwa akiishi
peke yake msituni
—katika shamba la
matunda.

Waache wale Bashani na
Gileadi^d kama ilivyokuwa
siku za kale.

- 15** “Kama ilivyokuwa katika

7:11 *Au labda, “amri itakuwa mbali sana.” 7:13 *Tnn., “kwa sababu ya ma-
tokeo ya matendo yao.”

SURA YA 7

a Zb 79:10
Zb 115:2
Yoe 2:17

b Isa 11:16
Isa 27:13
Ho 11:11

c Isa 40:11

d Yer 50:19
Eze 34:23

Safu ya 2

a Zb 78:12
Isa 63:11
Yer 23:7, 8

b Zb 126:2
Isa 26:11
Isa 66:18

c Isa 49:23

d Yer 33:9

e Kut 34:6, 7
Isa 1:18
Isa 44:22
Yer 50:20
Da 9:9

f Yer 23:3
Yoe 2:32

g Zb 103:9
Isa 57:16
Omb 3:22

h Kum 30:3
Zb 103:8, 13
Ho 2:19

i Zb 103:12
Isa 55:7
Yer 31:34

j Mwa 22:17
Zb 105:8-11
Lu 1:72, 73
Mdo 3:25, 26

siku ulizotoka nchini
Misri,

Nitamwonyesha yeye
mambo ya ajabu.^a

- 16** Mataifa yataona na kuai-
bika licha ya nguvu zote
walizo nazo.^b

Watafunika kinywa chao
kwa mkono wao;
Masikio yao yatakuwa ki-
ziwi.

- 17** Wataramba mavumbi
kama nyoka;^c

Kama wanyama wanaota-
mbaa wa duniani watato-
ka katika ngome zao wa-
kitetemeka.

Watakuja kwa Yehova Mu-
ngu wetu wakiwa na
hofu,

Nao watakuogopa wewe.”^d

- 18** Ni Mungu gani aliye kama
wewe,

Unayesamehe dhambi na
kuachilia makosa^e ya
watu waliobaki wa
urithi wako?^f

Hutaendelea kuwa na hasi-
ra milele,

Kwa maana unapendezwa
na upendo mshikama-
nifu.^g

- 19** Utatuonyesha tena rehe-
ma;^h utazishinda* dha-
mbi zetu.

Utazitupa dhambi zao
zote katika vilindi vya
bahari.ⁱ

- 20** Utamtendea Yakobo kwa
uaminifu,

Na Abrahamu kwa upendo
mshikamanifu,
Kama ulivyowaapia maba-
bu zetu tangu siku za
kale.^j

7:19 *Au “utazikanyaga-kanyaga chini;
utazitiisha.”

NAHUMU

YALIYOMO

- | | |
|--|---|
| <p>1 Mungu awalipiza kisasi maadui wake (1-7)
Mungu anataka watu wamwabudu yeye peke yake (2)
Yehova huwajali wanaomkimbilia (7)
Ninawi kuangamizwa (8-14)
Taabu haitatokea mara ya pili (9)
Taifa la Yuda latangaziwa habari njema (15)</p> | <p>2 Ninawi kuangamizwa (1-13)
“Malango ya mto yatafunguliwa” (6)</p> <p>3 “Ole kwa jiji la umwagaji wa damu.” (1-19)
Sababu za kuihukumu Ninawi (1-7)
Ninawi litaangamizwa kama No-amoni (8-12)
Ninawi halitaepuka kuangamizwa (13-19)</p> |
|--|---|

1 Tangazo dhidi ya Ninawi:^a Kitabu cha maono ya Nahumu* Mwelkoshi:

2 Yehova ni Mungu anayetaka watu wamwabudu yeye peke yake^b naye hulipiza kisasi;

Yehova hulipiza kisasi naye yuko tayari konyesha ghadhabu yake.^c

Yehova hulipiza kisasi dhidi ya maadui wake, Naye hukusanya ghadhabu kwa ajili ya maadui wake.

3 Yehova si mwepesi wa hasira,^d naye ana nguvu nyingi,^e

Lakini Yehova hatasita kamwe kutoa adhabu inayostahiliwa.^f

Kijia chake kimo katika upepo unaosababisha uharibifu na katika dhoruba,

Na mawingu ni mavumbi ya miguu yake.^g

4 Hukumea bahari,^h naye huikausha;
Naye huifanya mito yote ikauke.ⁱ

SURA YA 1

a Isa 10:12
Nah 3:7
Sef 2:13

b Kut 20:5

c Kum 32:35, 41
Isa 59:18

d Hes 14:18

e Ayu 9:4

f Kut 34:6, 7

g Ayu 38:1

h Ayu 38:11
Zb 104:6, 7
Zb 107:29

i Yos 3:16

Safu ya 2

a Isa 33:9
Amo 1:2

b 2Sa 22:8
Zb 68:7, 8

c Zb 97:4, 5
Isa 24:1

d Yer 10:10

e Kum 32:22

f Zb 136:1
Mt 19:17

g Zb 46:1
Zb 91:2
Met 18:10
Isa 25:4

h Zb 1:6

Bashani na Karmeli hunyauka,^a

Na maua ya Lebanoni hunyauka.

5 Milima hutetemeka kwa sababu yake,

Na vilima huyeyuka.^b

Dunia itasukasuka kwa sababu ya uso wake,

Pamoja na nchi na wote wanaoishi humo.^c

6 Ni nani anayeweza kusimama mbele ya hasira yake kali?^d

Na ni nani anayeweza kustahimili joto la hasira yake?^e

Ghadhabu yake itamwagwa kama moto,

Na miamba itavunjika-vunjika kwa sababu yake.

7 Yehova ni mwema,^f ni ngome katika siku ya taabu.^g

Anawakazia fikira* wale wanaotafuta kimbilio kwake.^h

8 Kwa mafuriko makubwa atapaangamiza kabisa mahali pake,*

1:7 *Au “Anawatunza.” Tnn., “Anawajua.” 1:8 *Yaani, Ninawi.

1:1 *Maana yake “Mfariji.”

Na giza litawafuatia maa-
dui wake.

- 9** Mtapanga njama gani dhi-
di ya Yehova?
Anasababisha maangamizi
kamili.
Taabu haitatokea tena
mara ya pili.^a
- 10** Kwa maana wamesokota-
na kama miiba,
Nao ni kama watu waliole-
wa pombe; *
Lakini watateketezwa ka-
bisa kama nyasi kavu.
- 11** Kutoka kwako atatoka
yule anayepanga njama
ya uovu dhidi ya Yehova,
Akitoa ushauri usiofaa.
- 12** Yehova anasema hivi:
“Ingawa walikuwa na ngu-
vu nyingi na walikuwa
wengi,
Hata hivyo, wataangami-
zwa na kutoweka. *
Nimekutesa wewe,[#] lakini
sitakutesa tena.
- 13** Na sasa nitavunja nira
yake na kuiondoa juu
yako,^b
Nami nitazikata pingu
zako vipande viwili.
- 14** Yehova ameamuru hivi ku-
kuhusu, *
‘Jina lako halitaendelezwa
tena.
Nitaziharibu sanamu zako
za kuchongwa na sana-
mu za chuma[#] kutoka
katika nyumba ya^Δ miu-
ngu yako.
Nitakuchimbia kaburi,
kwa sababu unachukiza.’
- 15** “Tazama! Miguu ya yule

1:10 *Au “pombe ya ngano.” 1:12 *Au labda, “naye atapita katikati yake.”
#Yaani, watu wa Yuda. 1:14 *Yaani, Ashuru. #Au “sanamu za kuyeyushwa.”
ΔAu “hekalu la.”

SURA YA 1

a Isa 10:24, 25

b Isa 14:25

Safu ya 2

a Isa 52:7
Ro 10:15

b Kum 16:16

SURA YA 2

c Yer 29:9

d 2Fa 17:6

anayeleta habari njema
iko milimani,
Yule anayetangaza amani.^a
Fanya sherehe zako,^b Ee
Yuda, timiza nadhiri
zako,
Kwa maana mtu asiyefaa
hatapita tena kati yako.
Ataangamizwa kabisa.”

- 2** Yule anayetawanya ame-
kuvamia. *^c
Linda ngome.
Linda njia.
Jitayarisheni[#] na mkusa-
nye nguvu zenu zote.
- 2** Kwa maana Yehova ataru-
disha fahari ya Yakobo,
Pamoja na fahari ya
Israeli,
Kwa sababu waangamizaji
wamewaangamiza;^d
Nao wameharibu machipu-
kizi yao.
- 3** Ngao za wanaume wake
hodari zimetwiwa rangi
nyekundu,
Mashujaa wake wamevaa
nguo nyekundu.
Vyuma vya magari yake ya
vita vinawakawaka kama
moto
Katika siku anayojitayari-
sha kwa ajili ya vita,
Na mikuki ya miberoshi
inapotikiswa.
- 4** Magari ya vita yanaende-
shwa kwa kasi sana bara-
barani.
Yanakimbia huku na huku
katika viwanja vya mji.
Yanang’aa kama mienge
inayowaka na kumweka
kama radi.
- 5** Atawaita maofisa wake.
Watajikwaa wanaposonga
mbele.

2:1 *Yaani, Ninawi. #Tnn., “Imarisheni viuno.”

Wanakimbilia haraka kwe-
nye ukuta wake;

Wanaweka kizuizi.

6 Malango ya mto yatafu-
nguliwa,
Na jumba la mfalme litaye-
yushwa.*

7 Imeamriwa:* Amefunu-
liwa,
Amechukuliwa, na vija-
kazi wake wanalia kwa
huzuni;

Wanalia kama njiwa huku
wakijipigapiga vifua.#

8 Katika siku zake zote jiji
la Ninawi^a lilikuwa kama
dimbwi la maji,
Lakini sasa wanakimbia.
“Simameni tuli! Simameni
tuli!”

Lakini hakuna yeyote ana-
yegeuka nyuma.^b

9 Poreni fedha, poreni dha-
habu!

Hazina zake haziishi.
Zimejazwa kila aina ya vitu
vyenye thamani.

10 Jiji liko tupu, liko ukiwa,
na limeharibiwa kabisa!^c
Mioyo yao inayeyuka kwa
woga, magoti yao yanale-
gea, viuno vyao vinatete-
meka;

Nyuso zao zote zimebadili-
ka rangi.

11 Liko wapi pango la simba,^d
mahali ambapo wanasim-
ba* wanakula,

Mahali ambapo simba ana-
toka akimwongoza mtoto
wake,

Na hakuna yeyote wa ku-
waogopesha?

12 Simba aliwararulia watoto

2:6 *Au “litaporomoka.” 2:7 *Au
“imeagizwa.” #Tnn., “mioyo.” 2:11
*Au “wanasimba wenye manyoya mare-
fu shingoni.”

SURA YA 2

a Mwa 10:8,11

b Sef 2:13

c Sef 2:15

d Yer 2:14, 15
Yer 50:17

Safu ya 2

a Isa 10:12

b Zb 46:9
Isa 37:24

c 2Fa 18:17

wake mawindo ya ku-
tosha,

Akayakaba pumzi mawi-
ndo kwa ajili ya majike
yake.

Alijaza mawindo katika
mapango yake,

Makao yake akayajaza wa-
nyama walioraruliwa.

13 “Tazama! Niko dhidi
yako,” asema Yehova
wa majeshi,^a

“Nitayateketeza kwa moto
magari yake ya vita,^b

Na upanga utawachinja
wanasimba wako.*

Nitayaangamiza kabisa
mawindo yako duniani,
Na sauti ya wajumbe wako
haitasikika tena.”^c

3 Ole kwa jiji la umwagaji
wa damu!

Limejaa kabisa udanganyi-
fu na unyang’anyi.

Halikosi kamwe mawindo!

2 Kuna sauti ya mjeledi na
mlio wa magurudumu,
Farasi anayekimbia kasi
na gari la vita linaloru-
karuka.

3 Mpanda farasi aliye juu ya
farasi, upanga unaomwe-
ka, na mkuki unaometa-
meta,

Umati wa watu waliouawa
na marundo ya maiti
—Maiti hazihesabiki.

Wanaendelea kujikwaa juu
ya maiti.

4 Yote hayo ni kwa sababu
ya matendo mengi ya
ukahaba yaliyotendwa
na huyo kahaba,
Aliye mrembo na mwenye
kuvutia, bimkubwa wa
uchawi,

2:13 *Au “wanasimba wako wenye ma-
nyoya marefu shingoni.”

Anayeyanasa mataifa kwa ukahaba wake na familia kwa uchawi wake.

- 5** “Tazama! Niko dhidi yako,”* asema Yehova wa majeshi,^a
 “Nitainua nguo yako juu na kufunika uso wako; Nitayafanya mataifa yaone uchi wako, Na falme zione aibu yako.

- 6** Nitatupa uchafu juu yako Na kukufanya udharau-liwe;

Nitakufanya uwe kioja.*^b

- 7** Kila mtu atakayekuona atakukimbia^c na kusema, ‘Jiji la Ninawi limeangami-zwa! Ni nani atakayelihurumia?’ Nitakutafutia wapi wafariji?

- 8** Je, wewe ni bora kuliko jiji la No-amoni,^{*d} lililoketi kando ya mifereji ya Nile?^e

Maji yalilizunguka; Utajiri wake ulikuwa bahari na ukuta wake ulikuwa bahari.

- 9** Nchi ya Ethiopia ilikuwa chanzo cha nguvu zake zisizo na mipaka, pia Misiri.

Putu^f na Walibya walikusaidia.^g

- 10** Lakini hata yeye alipele-kwa uhamishoni; Alienda utekwani.^h Watoto wake pia walipondwa-pondwa katika kila pembe ya barabara.

Walipiga kura ili kuwauza

3:5 *Yaani, Ninawi. 3:6 *Au “kitu cha kuchekesha.” 3:8 *Yaani, Thebesi.

SURA YA 3

a Nah 2:13

b Sef 2:15

c Nah 2:8

d Yer 46:25
Eze 30:14

e Isa 19:6

f Mwa 10:6

g 2Nya 16:8
Yer 46:8, 9

h Isa 20:4

Safu ya 2

a Zb 75:8
Yer 25:15

b 2Nya 32:3, 4

c Sef 2:13

d Kut 10:14, 15

wanaume wake wanao-heshimiwa,

Na wanaume wake wote wakuu wamefungwa kwa pingu.

- 11** Wewe pia utalewa;^a Utaenda mafichoni. Utatafuta kimbilio kutoka kwa adui.
- 12** Ngome zako zote ni kama mitini yenye tini za kwanza zilizoiva; Zikitikiswa, zitaanguka kinywani mwa walaji walafi.
- 13** Tazama! Wanajeshi wako ni kama wanawake kati yako. Malango ya nchi yako yatakuwa wazi kabisa kwa ajili ya maadui wako. Moto utateketeza kabisa makomeo ya malango yako.
- 14** Teka maji kabla hujazingi-rwa!^b Imarisha ngome zako. Shuka chini kwenye matope na kukanyagakanyaga udongo wa mfinyanzi; Chukua chombo cha kufyatulia matofali.
- 15** Hata huko moto utakuteketeza kabisa. Upanga utakukatakata.^c Utakutafuna kama nzige wachanga wanavyofanya.^d Ongezeka sana kama nzige wachanga! Naam, ongezeka sana kama nzige!
- 16** Umezidisha wafanyabiashara wako kuliko nyota za mbinguni. Nzige mchanga hujivua ngozi kisha huruka na kwenda zake.

1521

- 17 Walinzi wako ni kama nzige,
Na maafisa wako ni kama kundi la nzige.
Wanapiga kambi katika mazizi ya mawe siku yenye baridi,
Lakini jua linapowaka, wao huruka na kwenda zao;
Na hakuna yeyote anayejua mahali walipo.
- 18 Wachungaji wako wanasi-nzia, Ee mfalme wa Ashuru;
Wakuu wako wanakaa katika makao yao.

Safu ya 2

SURA YA 3

a Nah 2:8

b Sef 2:15

c Isa 10:5, 6
Isa 37:18

NAHUMU 3:17 – HABAKUKI 1:3

- Watu wako wametawanyi-ka milimani,
Na hakuna yeyote anayewakusanya pamoja.^a
- 19 Msiba wako hauna kitulizo.
Jeraha lako haliwezi kuponywa.
Wale wote wanaosikia habari zako watapiga makofi;^b
Kwa maana ni nani ambaye hajateseka kwa saba bu ya ukatili wako usio na mwisho?”^c

HABAKUKI

YALIYOMO

- 1 Nabii alilia msaada (1-4)
‘Ee Yehova, mpaka lini?’ (2)
“Kwa nini unavumilia ukandamizaji?” (3)
Wakaldayo, watumiwa na Mungu kutekeleza hukumu (5-11)
Nabii amsihi Yehova (12-17)
‘Mungu wangu, wewe hufi’ (12)
‘Wewe ni safi sana usiweze kutazama uovu’ (13)
- 2 ‘Nitakaa macho kuhusu atakalosema’ (1)

- Yehova amjibu nabii (2-20)
‘Endelea kutarajia maono’ (3)
Mwadilifu ataishi kwa uaminifu (4)
Ole tano kwa Wakaldayo (6-20)
Dunia yote itajaa ujuzi kumhusu Yehova (14)
- 3 Nabii asali ili Yehova achukue hatua (1-19)
Mungu atawaokoa watiwa-mafuta wake (13)
Nitashangilia katika Yehova (17, 18)

1 Tangazo ambalo nabii Habakuki* alipokea katika maono:

- 2 Ee Yehova, nililie msaada mpaka lini, lakini wewe hunisikii?^a

1:1 *Huenda jina hili linamaanisha “Kumbatio Changamfu.”

SURA YA 1

a Zb 13:1

Safu ya 2

a Zb 22:1
Zb 74:10
Ufu 6:10

Nitaomba msaada kwa saba bu ya ukatili mpaka lini, lakini huingilii kati?^a

- 3 Kwa nini unanifanya nione mambo mabaya?
Na kwa nini unavumilia ukandamizaji?

1:2 *Au “huniokoi.”

Kwa nini uharibifu na ukatili uko mbele yangu?

Na kwa nini ugomvi na mizozo inaongezeka?

4 Kwa hiyo sheria haifanyi kazi,

Na haki haitekelezwi kamwe.

Kwa maana mwovu amezingira mwadilifu; Ndiyo sababu haki imepotoshwa.^a

5 “Tazameni miongoni mwa mataifa, kazeni uangalifu!

Tazameni kwa mshangao na kustaajabu;

Kwa maana jambo fulani litatukia katika siku zenu

Ambalo hamtaamini hata mkiambiwa.^b

6 Kwa maana tazama, ninawainua Wakaldayo,^c

Taifa katili na linalotenda haraka-haraka,

Wanasambaa upesi katika maeneo makubwa sana ya dunia

Ili wachukue kwa nguvu makao ambayo si yao.^d

7 Wanatisha na kuogopesha. Wanaweka sheria* yao wenyewe na mamlaka# yao wenyewe.^e

8 Farasi wao wanakimbia kasi kuliko chui,

Nao ni wakali kuliko mbwamwitu wakati wa usiku.^f

Farasi wao wa vita hukimbia mbele kwa kasi;

Farasi wao hutoka mbali sana.

Wanashuka chini kwa kasi kama tai anayekimbilia chakula.^g

SURA YA 1

a Ayu 12:6
Zb 12:8
Mhu 8:11
Isa 1:21
Mdo 7:52, 53

b Isa 28:21
Isa 29:14
Omb 4:11, 12
Mdo 13:40, 41

c Yer 22:7
Yer 46:2

d Kum 28:49-51
Yer 5:15-17
Yer 6:22, 23
Eze 23:22, 23

e Yer 39:5-7
Da 5:18, 19

f Yer 5:6

g Yer 4:13
Omb 4:19
Eze 17:3

Safu ya 2

a Yer 25:9

b Isa 27:8
Eze 17:10

c 2Fa 24:12

d Yer 32:24
Yer 52:7

e Isa 47:5, 6
Yer 51:24
Zek 1:15

f Da 5:1, 4

g Zb 90:2
Zb 93:2
Ufu 1:8

h 1Ti 1:17
Ufu 15:3

i Kum 32:4

j Yer 30:11

k Zb 5:4, 5

l Yer 12:1

m Zb 35:21, 22

9 Wote huja wakikusudia kutenda ukatili.^a

Nyuso zao kwa pamoja ni kama upepo wa mashariki,^b

Na o huchota mateka kama mchanga.

10 Wanawadhikahi wafalme Na kuwacheka maofisa wakuu.^c

Wanaicheka kila ngome;^d Wanatengeneza daraja kwa rundo la udongo na kuiteka.

11 Kisha wanasonga mbele kama upepo na kupita humo,

Lakini watakuwa na hatia,^e Kwa sababu wanasema nguvu zao zinatoka kwa mungu wao.^{**f}

12 Je, wewe si wa tangu milele, Ee Yehova?^g

Ee Mungu wangu, Mtakati-fu wangu, wewe hufi.^{*h}

Ee Yehova, uliwachagua ili watekeleze hukumu;

Mwamba wangu,ⁱ uliwa-weka ili watekeleze adhabu.^{#j}

13 Macho yako ni safi sana yasiweze kutazama uovu, Nawe huwezi kuvumilia uovu.^k

Basi, kwa nini unawavumilia wenye hila^l

Na kunyamaza mtu mwovu anapomweza mtu mwadilifu kuliko yeye?^m

14 Kwa nini unamfanya mwanaadamu awe kama samsaki wa baharini, Kama viumbe wanaotambaa ambao hawana mtawala?

1:11 *Au labda, “nguvu zao ni mungu wao.” **1:12** *Au labda, “sisi hatutaku-fa.” #Au “wakaripie.”

1:7 *Au “haki.” #Au “heshima.”

- 15** Hao wote yeye* huwavua kwa ndoano. Huwakamata kwa wavu wake wa kukokotwa, Naye huwakusanya katika wavu wake wa kuvulia samaki. Ndiyo sababu anashangilia sana.^a
- 16** Ndiyo sababu anatoa dhabihu kwa ajili ya wavu wake wa kukokotwa Na kutoa dhabihu* kwa ajili ya wavu wake wa kuvulia samaki; Kwa maana nyavu hizo zimeletea utajiri,[#] Na chakula chake ni bora.
- 17** Je, ataendelea kutoa samaki katika wavu wake wa kukokotwa?* Je, ataendelea kuyaangamiza mataifa bila huruma?^b
- 2** Nitaendelea kusimama katika kituo changu cha ulinzi,^c Nami nitasimama juu ya boma. Nitaendelea kukaa macho ili nione atakalosema kupitia kwangu Na lile nitakalojibu nitakapokaripiwa.
- 2** Kisha Yehova akanijibu: “Andika maono haya, na uyaandike waziwazi kwenye mabamba,^d Ili anayeyasoma kwa sauti, ayasome kwa urahisi.*^e
- 3** Kwa maana maono hayo bado yatatimia kwa wakati wake uliowekwa,

1:15 *Yaani, jeshi la Wakaldayo. 1:16 *Au “kufukiza moshi wa dhabihu.” #Tnn., “Kwa maana kupitia hizo fungu lake limetiwa mafuta mengi.” 1:17 *Au labda, “kuchomoa upanga wake.” 2:2 *Au “kwa ufasaha.”

SURA YA 1

a Yer 50:11

b 2Nya 36:17

Nah 3:7

SURA YA 2

c Isa 21:8

Mik 7:7

d Kut 17:14

e Kum 31:9, 11

Safu ya 2

a Mik 7:7

b Yoh 3:36

Ro 1:17

Gal 3:11

Ebr 10:38

c Isa 14:16, 17

d Isa 14:4

e Yer 51:11

Nayo yanasonga haraka kuelekea mwisho* wake, nayo hayatasema uwongo.

Hata yakikawia,[#] endelea kuyatarajia!^{△a}

Kwa maana hakika yatatimia.

Hayatachelewa!

4 Mwangalie mtu mwenye kiburi;*

Hana unyoofu ndani yake. Lakini mwadilifu ataishi kwa uaminifu wake.^{#b}

5 Kwa kweli, kwa sababu divai ina hila,

Mtu mwenye kiburi hatatimiza lengo lake.

Hufanya hamu* yake iwe kubwa kama Kaburi;#

Yeye ni kama kifo na hawezi kutoshelezwa.

Huendelea kuyakusanya mataifa yote

Na kujikusanyia watu wa mataifa yote.^c

6 Je, hao wote hawatasema methali, fumbo, na vitendawili kumshutumumu?^d

Watasema:

‘Ole wake anayejirundikia vitu visivyo vyake

—Mpaka lini?—

Na kufanya deni lake mwenyewe liwe kubwa hata zaidi!

7 Je, wanaokudai hawatainuka kwa ghafla?

Wataamka na kukutikisa kwa fujo,

Nawe utakuwa kitu cha kuporwa nao.^e

2:3 *Au “utumizo.” #Au “Hata ikionekana kwamba yanakawia.” [△]Au “kuyangojea kwa hamu!” 2:4 *Au “Tazama! Nafsi yake imefutuka.” #Au labda, “imani yake; itikadi yake.” 2:5 *Au “nafsi.” #Au “Sheoli.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

- 8** Kwa sababu ulipora mataifa mengi,
Mataifa mengine yote yatakupora,^a
Kwa sababu ulimwaga damu ya wanadamu
Na kwa sababu ya ukatili ulioitendea dunia,
Majiji na wale wanaoishi humo.^b
- 9** Ole wake anayeitafutia nyumba yake faida ya uovu,
Ili aweke kiota chake juu,
Aepuke kunaswa na msiba!
- 10** Umepanga njama ya aibu dhidi ya nyumba yako.
Kwa kuyaangamiza mataifa mengi unatenda dhambi dhidi yako mwenyewe.*^c
- 11** Kwa maana jiwe litapaza sauti kutoka ukutani,
Na kutoka kwenye mbaao za paa, boriti italijibu jiwe hilo.
- 12** Ole wake anajejenga jiji kwa umwagaji wa damu,
Na kuusimamisha mji kwa ukosefu wa uadilifu!
- 13** Tazama! Je, si Yehova wa majeshi anayesababisha mataifa yafanye kazi kwa bidii ili kuulisha moto,
Na kusababisha mataifa yajichoshe bure?^d
- 14** Kwa maana dunia itajaa ujuzi wa utukufu wa Yehova
Kama maji yanavyoifunika bahari.^e
- 15** Ole wake anayewapa wenzake kinywaji,
Na kuongeza ghadhabu na hasira ndani yake ili awalweshe,
Kusudi atazame uchi wao!

2:10 *Au "dhidi ya nafsi yako."

SURA YA 2

a Isa 13:19
Yer 27:6,7
Zek 2:7-9

b 2Nya 36:17
Zb 137:8

c Isa 14:20

d Yer 51:58

e Zb 72:19
Isa 11:9
Zek 14:9

Safu ya 2

a Zb 75:8
Isa 51:22,23
Yer 25:28
Yer 51:57

b Zb 137:8
Yer 50:28
Yer 51:24

c Isa 42:17
Isa 44:19,20
Isa 45:20

d Isa 40:19
Isa 46:6

e Yer 51:17

f Isa 6:1

- 16** Utajaa kabisa aibu badala ya utukufu.

Wewe pia—kunywa na kufunua hali yako ya kuto-tahiriwa.*

Kikombe kilicho kwenye mkono wa kuume wa Yehova kitzunguka na kufika kwako,^a

Na fedheha itafunika kabisa utukufu wako;

- 17** Kwa sababu ukatili ulioitendea Lebanoni utakufunika,

Na maangamizi yaliyowati-sha wanyama yatakuja,

Kwa sababu ulimwaga damu ya wanadamu

Na kwa sababu ya ukatili ulioitendea dunia,

Uliyoyatendea majiji na wale wanaoishi humo.^b

- 18** Sanamu ya kuchongwa ina faida gani

Na mtu ndiye aliyechonga?

Sanamu ya chuma* na mwalimu wa uwongo ana faida gani,

Hata ingawa yule aliyeyite-ngeneza anaitumaini,
Akitengeneza miungu ya ubatili ambayo haiwezi kuongea?^c

- 19** Ole wake anayekiambia kipande cha ubao, "Amka!"
Au anayeliambia jiwe lisi-loweza kuongea, "Amka! Tufundishe!"

Tazama! Sanamu hiyo imefunikwa kwa dhahabu na fedha,^d

Nayo haina pumzi yoyote ndani yake.^e

- 20** Lakini Yehova yuko katika hekalu lake takatifu.^f

2:16 *Au labda, "na kupepesuka." 2:18

*Au "sanamu ya kuyeyushwa."

Dunia yote na inyamaze mbele zake!"^a

3 Sala ya nabii Habakuki, aliyoitoe kama nyimbo za huzuni:*

2 Ee Yehova, nimesikia habari kukuhusu.

Ninaogopa matendo yako, Ee Yehova.

Uyafufue kati ya ile miaka!*

Uyafanye yajulikane kati ya hiyo miaka.*

Nawe ukumbuke kuonyesha rehema wakati wa msukusuko.^b

3 Mungu alikuja kutoka Temani,

Yeye Aliye Mtakatifu kutoka Mlima Parani.^c (*Sela*)*

Utukufu wake ulifunika mbingu;^d

Na dunia ikajaa sifa yake.

4 Aling'aa kama nuru.^e

Miale miwili ilimweka kutoka mkononi mwake, Ambamo nguvu zake zilikuwa zimefichika.

5 Ugonjwa hatari ulitangulia mbele zake,^f

Na homa kali ilimfuata miuguuni.

6 Alisimama tuli na kuitikisa dunia.^g

Alitazama mara moja tu, akayafanya mataifa yaru.^h

Milima ya milele ikavunjwawunjwa,

Na vilima vya kale vikainama chini.ⁱ

Vijia vya zamani za kale ni vyake.

7 Nyliona taabu katika mahema ya Kushani.

SURA YA 2

a Zb 76:8
Zb 115:3
Zek 2:13

SURA YA 3

b Omb 3:32

c Kum 33:2
Amu 5:4
Zb 68:7,8

d Kut 19:16

e Kut 13:21

f Hes 14:11,12
Hes 16:46
Hes 25:1,9

g Isa 13:13
Hag 2:21

h Kut 14:25
Kut 23:27

i Zb 114:1,4
Nah 1:5

Safu ya 2

a Kut 15:14,15
Hes 22:3,4

b Zb 114:1,3
Isa 50:2
Nah 1:4

c Kum 33:26

d Zb 68:17

e Kut 19:18
Zb 114:1,4

f Zb 77:16

g Yos 10:12

h Zb 77:17,18

Vitambaa vya mahema ya nchi ya Midiani vilitetemekela.^a

8 Je, umeikasirikia mito, Ee Yehova,

Je, hasira yako inawaka dhidi ya mito?

Au unaikasirikia vikali bahari?^b

Kwa sababu ulipanda farasi wako;^c

Magari yako ya vita yalishinda.*^d

9 Upinde wako umefunuliwa na uko tayari.

Fito zimepewa* kazi kwa kiapo.*^e (*Sela*)

Unaipasua dunia kwa mito.

10 Milima ilipindapinda kwa maumivu ilipokuona.^e

Mvuva kubwa ilinyesha nchini.

Kilindi cha maji kilinguruma kwa sauti yake.^f

Kikainua mikono yake juu.

11 Jua na mwezi vilisimama tuli kwenye makao yake yaliyo juu sana.^g

Mishale yako ilitoka kama nuru.^h

Radi ya mkuki wako ilikuwa nyangavu.

12 Ulipiga mwendo duniani kwa ghadhabu.

Ukayakanyaga-kanyaga* mataifa kwa hasira.

13 Ulitoka ili kuwaokoa watu wako, kumwokoia mtiwamafuta wako.

Ulimpondaponda kiongozi wa* nyumba ya waovu.

3:8 *Au "yalikuwa wokovu." **3:9** *Au labda, "Mishale imepewa." **3:12** *Tnn., "Ukayapura." **3:13** *Tnn., "Ulikipondaponda kichwa cha."

3:1 *Au "nyimbo za maombolezo." **3:2** *Au labda, "wakati wetu!" **3:3** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

Ilifunuliwa wazi kuanzia
kwenye msingi hadi juu.*
(Sela)

- 14 Uliwachoma vichwa ma-
shujaa wake kwa silaha*
zake mwenyewe

Walipoondoka kwa kishi-
ndo ili kunitawanya.

Walishangilia sana ku-
mnyafua kisiri mtu
anayeteseka.

- 15 Ulivuka bahari kwa farasi
wako,
Katikati ya mawimbi yali-
yoinuka ya maji mengi.

- 16 Nilisikia nikatetemeka
kwa ndani;*
Niliposikia sauti hiyo mi-
domo yangu ilitetemeka.
Uozo ukaingia mifupani
mwangu;^a
Miguu yangu ikatetemeka.
Lakini nangojea kimya-
kimya ile siku ya taabu,^b

3:13 *Tnn., “shingoni.” 3:14 *Tnn.,
“fito.” 3:16 *Tnn., “na tumbo langu li-
katetemeka.”

SURA YA 3

a Zb 119:120
Yer 23:9
Da 8:27

b Zb 42:5
Isa 26:20
Omb 3:26

Safu ya 2

a Kut 15:2
Isa 2:1
Zb 18:2
Zb 27:1
Isa 61:10

b Isa 12:2
Flp 4:13

c 2Sa 22:34

Kwa sababu inawajia watu
wanaotushambulia.

- 17 Ingawa huenda mtini usi-
chanue,
Na huenda mizabibu isiwe
na matunda;
Ingawa huenda mizeituni
isizae,
Na mashamba yasiwe na
mazao yoyote;
Ingawa huenda mazizi ya-
siwe na kondoo,
Na mabanda yasiwe na
ng'ombe;
- 18 Lakini mimi nitashangilia
katika Yehova;
Nitakuwa na shangwe ka-
tika Mungu wa wokovu
wangu.^a
- 19 Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova ni nguvu zangu;^b
Ataifanya miguu yangu iwe
kama ya paa
Na kuniwezesha kutembea
mahali palipoinuka.^c

Kwa kiongozi;
kwa kutumia vinanda vyangu.

SEFANIA

YALIYOMO

- Siku ya Yehova ya hukumu iko
karibu (1-18)
Siku ya Yehova inakuja haraka
sana (14)
Fedha na dhahabu haviwezi
kuokoa (18)
- Mtafuteni Yehova kabla ya siku yake
ya hasira (1-3)
Tafuteni uadilifu na upole (3)
“Huenda mtafichwa” (3)
Mataifa jirani yahukumiwa (4-15)
- Yerusalemu, jiji lenye uasi na
upotovu (1-7)

Kuhukumiwa na kurudishwa (8-20)
Wapewa lugha safi (9)
Wanyenyekevu na wapole
wataokolewa (12)
Yehova atashangilia kwa sababu
ya Sayuni (17)

1 Neno la Yehova lililomjia Sefania* mwana wa Kushi mwana wa Gedalia mwana wa Amaria mwana wa Hezekia katika siku za Yosia^a mwana wa Amoni^b mfalme wa Yuda:

2 "Nitafagilia mbali kabisa kila kitu kutoka katika nchi," asema Yehova.^c

3 "Nitamfagilia mbali mwanaadamu na mnyama. Nitamfagilia mbali ndege wa angani na samaki wa baharini,^d

Na pia vitu vinavyokwaza*^e pamoja na waovu;

Nami nitawaondoa wanadamu kutoka katika nchi," asema Yehova.

4 "Nitaunyoosha mkono wangu dhidi ya watu wa Yuda

Na dhidi ya wakaaji wote wa Yerusalemu,

Nami nitafutulia mbali kutoka mahali hapa kila kitu kinachohusiana na* Baali,^f

Jina la makuhani wa miungu ya kigeni pamoja na makuhani wenyewe,^g

5 Na wale wanaoliinamia jeshi la mbinguni wakiwa juu ya paa,^h

Na wale wanaoinama chini na kuapa kwamba watakuwa washikamani-fu kwa Yehovaⁱ

Na wakati uleule wakiapa kwamba watakuwa washikamanifu kwa Malkamu;

SURA YA 1

a 2Fa 22:1, 2
Yer 1:2

b 2Fa 21:18-20

c 2Fa 22:16
Isa 6:11
Yer 6:8

d Yer 4:25

e Eze 14:3

f Hes 25:3
Amu 2:11, 13
2Nya 28:1, 2
Yer 11:17

g 2Fa 23:5

h 2Nya 33:1, 3
Yer 19:13

i Isa 48:1

j Yos 23:6, 7
1Fa 11:33
Yer 49:1

Safu ya 2

a Isa 1:4
Yer 2:13

b Isa 43:22

c Yoe 2:1
2Pe 3:10

d 2Fa 25:7
Yer 39:6

e 2Nya 33:1, 14
Ne 3:3
Ne 12:38, 39

f 2Nya 34:22

6 Na wale wanaogeuka na kuacha kumfuata Yehova^a

Na wale wasiomtafuta Yehova wala kuomba ushauri wake."^b

7 Nyamazeni mbele za Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, kwa maana siku ya Yehova iko karibu.^c

Yehova ametayarisha dhahibi; amewatakasa wale aliowaalika.

8 "Katika siku ya dhahibi ya Yehova nitawafanya wakuu wawajibike, Wana wa mfalme,^d na wote wanaovaa mavazi ya kigeni.

9 Siku hiyo nitamfanya kila mtu anayepanda jukwaa-ni* awajibike,

Wale wanaojaza nyumba ya bwana wao ukatili na udanganyifu.

10 Siku hiyo," asema Yehova, "Kutakuwa na sauti ya kilio kwenye Lango la Samaki,^e

Mayowe katika Wilaya ya Pili ya jiji,^f

Na mshindo mkubwa vilimani.

11 Pigeni mayowe, enyi wakaaji wa Makteshi,*

Kwa maana wafanyabishara wote wameangamizwa;^g

Wote wanaopima fedha wameuawa.

12 Wakati huo nitatumia taa kupekua Yerusalemu kwa makini,

1:1 *Maana yake "Yehova Ameficha (Amesitiri Kama Hazina)." 1:3 *Inaonekana kwamba ni vitu au mambo yanayohusiana na ibada ya sanamu. 1:4 *Au "dalili yoyote ya."

1:9 *Au "kwenye kizingiti." Labda ni juu kwa kiti cha mfalme. 1:11 *Inaonekana ni eneo la Yerusalemu lililokuwa karibu na Lango la Samaki. # Tnn., "wamenyamazishwa."

Nami nitawafanya
wasiojali* wawajibike,
wanaosema moyoni
mwao,
‘Yehova hatatenda mema,
wala hatatenda mabaya.’^a

13 Utajiri wao utaporwa na
nyumba zao zitaharibiwa
kabisa.^b

Watajenga nyumba, lakini
hawatakaa ndani yake;
Nao watapanda mashamba
ya mizabibu, lakini
hawatakunywa divai
yake.^c

14 Ile siku kuu ya Yehova iko
karibu!^d

Iko karibu, nayo inakuja
haraka sana!^{*e}
Sauti ya siku ya Yehova ni
chungu.^f

Siku hiyo shujaa atalia
kwa sauti.^g

15 Siku hiyo ni siku ya gha-
dhabu,^h

Siku ya taabu na maumivu
makali,ⁱ

Siku ya dhoruba na ukiwa,
Siku ya giza na utusitusi,^j

Siku ya mawingu na utusi-
tusi mzito,^k

16 Siku ya pembe na ya kele-
le za vita,^l

Dhidi ya majiji yenye ngo-
me na dhidi ya minara
mirefu ya pembeni.^m

17 Nitawataabisha wana-
damu,

Nao watatembea kama vi-
pofu,ⁿ

Kwa sababu wamemtendea
Yehova dhambi.^o

1:12 *Tnn., “wanaoganda juu ya machi-
cha yao,” kana kwamba wamo ndani ya
mtungi wa kushinikizia divai. **1:14** *Au
“inakuja kwa kasi sana!”

SURA YA 1

a Zb 10:13
Zb 14:1

b Isa 6:11

c Kum 28:30
Yer 5:17

d Yoe 2:1

e Hab 2:3

f Isa 66:6

g Isa 33:7
Yoe 1:15

h Ufu 6:17

i Yer 30:7

j Amo 5:18, 20
Mdo 2:20

k Yoe 2:2

l Yer 4:19

m Isa 2:12, 15

n Kum 28:28, 29
Isa 59:9, 10

o Isa 24:5
Da 9:5, 8

Safu ya 2

a Zb 79:2, 3
Yer 9:22
Yer 16:4

b Met 11:4
Isa 2:20
Eze 7:19

c Kum 32:22
Yer 7:20

d Yer 4:27

SURA YA 2

e Yoe 1:14
Yoe 2:15, 16

f Isa 1:4
Yer 6:15

g 2Fa 23:26
2Nya 36:16, 17
Yer 23:20
Omb 4:11

h Isa 55:6
Amo 5:6

i Mwa 7:13, 16
Isa 26:20
Yoe 2:12, 14
Amo 5:15

j Yer 47:5

Damu yao itamwagwa
kama mavumbi,
Na nyama* yao kama
mavi.^a

18 Fedha yao wala dhahabu
yao haitaweza kuwaokoa
katika siku ya ghadhabu
ya Yehova;^b

Kwa maana dunia yote ita-
teketezwa kwa moto wa
bidii yake.^c

Kwa sababu atawaangami-
za kabisa wakaaji wote
wa dunia, kwa kweli ya-
takuwa maangamizi ye-
nye kutisha.”^d

2 Kusanyikeni pamoja,
naam, jikusanyeni,^e

Ewe taifa lililoona aibu.^f

2 Kabla amri haijateke-
lezwa,

Kabla siku hiyo haijapepe-
ruka kama makapi,

Kabla hasira inayowaka
ya Yehova haijaja juu
yenu,^g

Kabla siku ya hasira
ya Yehova haijaja juu
yenu,

3 Mtafuteni Yehova,^h ninyi
nyote mlio wapole* wa
dunia,

Mnaoshika amri zake za
uadilifu.[#]

Utafuteni uadilifu, utafu-
teni upole.[△]

Huenda[□] mtafichwa katika
siku ya hasira ya Yehova.ⁱ

4 Kwa maana Gaza litakuwa
jiji lililoachwa mahame;
Na Ashkeloni litafanywa
ukiwa./

Waashdodi watafukuzwa

1:17 *Tnn., “matumbo.” **2:3** *Au “wa-
nyenyekevu.” #Tnn., “hukumu yake.”

△Au “unyenyekevu.” □Au “Inaelekea.”

kweupe kabisa wakati wa mchana,*

Na Ekroni litang'olewa.^a

- 5 “Ole kwa wale wanaokaa pwani, taifa la Wakere-thi!^b

Neno la Yehova liko dhidi yenu.

Ee Kanaani, nchi ya Wafilisti, nitakuangamiza, Hivi kwamba hakuna mkaaji atakayebaki.

- 6 Na eneo la pwani litakuwa eneo la malisho, Lenye visima kwa ajili ya wachungaji na mazizi ya mawe kwa ajili ya kondo.

- 7 Litakuwa eneo la watu waliobaki wa nyumba ya Yuda;^c

Watalisha huko.

Jioni watalala chini katika nyumba za Ashkeloni.

Kwa maana Yehova Mungu wao atawaelekezea uangalifu,*

Naye atawakusanya na kuwarudisha mateka wao.^d

- 8 “Nimesikia shutuma za Moabu^e na matusi ya Waamoni,^f

Ambao wamewadhikaki watu wangu na kujigamba kwa vitisho dhidi ya eneo lao.^g

- 9 Kwa hiyo, kwa hakika kama ninavyoishi,” asema Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, “Moabu itakuwa tu kama Sodoma,^h

Na Waamoni kama Gomora,ⁱ

Mahali penye upupu, shi-

2:4 *Au “aduhuri.” 2:7 *Au “atawataunza.”

SURA YA 2

a Yer 25:17, 20
Amo 1:6-8
Zek 9:5, 6

b Eze 25:16, 17

c Isa 11:11
Yer 31:7
Hag 1:12

d Zb 126:1
Yer 23:3
Eze 39:25
Amo 9:14
Mik 2:12
Mik 4:10
Sef 3:20

e Yer 48:26, 27
Eze 25:8, 9

f Yer 49:1
Eze 25:3

g Zb 83:2, 4

h Eze 25:11
Amo 2:1, 2

i Mwa 19:24, 25

Safu ya 2

a Amo 1:13-15
Yud 7

b Isa 16:6
Yer 48:29

c Zb 22:27
Mal 1:11

d Isa 43:3
Eze 30:4, 5

e Nah 3:7

mo la chumvi, na nchi iliyoachwa ukiwa milele.^a

Watu wangu waliobaki watawapora,

Na watu waliobaki wa taifa langu watamiliki nchi yao.

- 10 Hayo ndiyo watakatayopata badala ya kiburi chao,^b Kwa sababu waliwadhihaki na kujikweza dhidi ya watu wa Yehova wa majeshi.

- 11 Yehova atawaogopesha sana;* Kwa maana ataiharibu kabisa[#] miungu yote ya dunia,

Na visiwa vyote vya mataifa vitamwinamia,^{Δc} Kila kisiwa kikiwa mahali pake.

- 12 Ninyi Waethiopia mtauawa pia kwa upanga wangu.^d

- 13 Ataunyoosha mkono wake kuelekea kaskazini na kuangamiza Ashuru, Naye atalifanya Ninawi liwe ukiwa,^e liwe kavu kama jangwa.

- 14 Mifugo italala ndani yake, kila aina ya wanyama wa mwituni.*

Mwari na nungunungu watalala usiku kati ya nguzo zake zilizoanguka.

Sauti itaimba dirishani. Kutakuwa na uharibifu kwenye kizingiti;

Kwa maana atafunua mpao za mierezi zinazopamba kuta.

2:11 *Au “atawatisha.” #Au “ataidhoo-fisha.” ΔAu “vitamwabudu.” 2:14 *Tnn., “kila mnyama wa mwituni katika taifa.”

15 Hili ndilo jiji lenye kiburi lililokuwa likikaa kwa usalama, Lililokuwa likisema moyoni mwake, 'Mimi ndiye, na hakuna mwingine yeyote.' Jinsi ambavyo limekuwa kitu chenye kutisha, Mahali ambapo wanyama wa mwituni wanalala! Kila mtu anayepita karibu nalo atapiga mluzi na kukitisa ngumi yake."^a

3 Ole kwa jiji lenye uasi, lenye uchafu, lenye ukandamizaji!^b

2 Halijatii sauti yoyote;^c halijakubali nidhamu yoyote.^d

Halijamtumaini Yehova;^e halijamkaribia Mungu wake.^f

3 Wakuu wake walio ndani yake ni simba wanaonguruma.^g

Waamuzi wake ni mbwamwitu wakati wa usiku; Hawaachi hata mfupa mmoja wa kuguguna mpaka asubuhi.

4 Manabii wake ni wakaidi, wanaume wenye hila.^h Makuhani wake wanachafua kilicho kitakatifu;ⁱ Wanaitendea sheria kikatili.^j

5 Yehova ni mwadilifu miongoni mwake;^k hatendi kosa lolote. Asubuhi baada ya asubuhi hutangaza hukumu zake,^l

Kama nuru ya mchana isivyokosa kuangaza. Lakini asiye mwadilifu haoni aibu hata kidogo.^m

SURA YA 2
a Nah 3:1,19

SURA YA 3
b Isa 5:7
Yer 6:6

c Yer 22:21
Yer 32:23

d Zb 50:17
Isa 1:5
Yer 5:3

e Zb 78:22
Yer 17:5

f Isa 29:13

g Isa 1:23
Eze 22:27

h Omb 2:14

i Yer 23:11

j Eze 22:25, 26
Mik 3:9

k Kum 32:4

l Yer 21:12

m Yer 3:3
Yer 8:12
Sef 2:1

Safu ya 2
a Law 18:28

b Isa 5:3, 4
Isa 63:8
2Pe 3:9

c Yer 7:5-7
Yer 25:5, 6

d Mik 2:1

e Zb 37:34
Zb 130:7
Isa 30:18

f Isa 34:2
Yoe 3:2
Ufu 16:14
Ufu 19:19

g Eze 36:5

h Zek 8:23

6 "Niliyaangamiza mataifa; minara yao ya pembeni iliachwa ukiwa.

Nilihariibu barabara zao, hivi kwamba hakuna yeyote aliyepita.

Majiji yao yaliachwa magofu, bila mtu yeyote, bila mkaaaji yeyote.^a

7 Nikasema, 'Hakika mtanionogopa na kukubali nidhamu,'^{*b}

Ili makao yake yasiweze kuharibiwa^c

—Ni lazima nilifanye liwajibike[#] kwa sababu ya mambo hayo yote.

Lakini walitamani hata zaidi kutenda kwa upotovu.^d

8 'Kwa hiyo endeleeni kunitarajia,'^{**e} asema Yehova,

'Mpaka siku nitakapoinuka ili kuchukua nyara,[#]

Kwa maana uamuzi wangu wa hukumu ni kuyakusanya mataifa, kuzikusanya nyama falme,

Niwamwagie ghadhabu yangu, hasira yangu yote inayowaka;^f

Kwa maana dunia yote itateketzwa kwa moto wa bidii yangu.^g

9 Kwa maana wakati huo nitabadilii lugha ya mataifa iwe lugha safi,

Ili wote waweze kuliitia jina la Yehova,

Wamtumikie bega kwa bega.^{***h}

10 Kutoka eneo la mito ya Ethiopia,

3:7 *Au "kurekebisha." #Au "niliadhibu." 3:8 *Au "kuningojea kwa subira." #Au labda, "nitakapoinuka nikiwa shahidi." 3:9 *Au "wamwabudu kwa umoja."

Wale wanaonisihi, binti
ya watu wangu waliota-
wanywa, wataniletea za-
wadi.^a

- 11** Siku hiyo hamtaibishwa
Kwa sababu ya matendo
yenu yote ya uasi mliyo-
nitendea,^b

Kwa maana wakati huo
nitawaondoa kati yenu
watu wenye kiburi wa-
naojigamba;
Nanyi hamtakuwa tena na
kiburi katika mlima wa-
ngu mtakatifu.^c

- 12** Nitawaruhusu watu wa-
nyenyekevu na wapole
wabaki miongoni
mwenu,^d

Nao watapata kimbilio
katika jina la Yehova.

- 13** Waisraeli watakaobaki^e
hawatatenda mambo
yasiyo ya uadilifu;^f

Hawatasema uwongo, wala
hawatakuwa na ndimi za
udanganyifu vinywani
mwao;

Watakula* na kulala, na
hakuna yeyote atakaye-
waogopesha.^g

- 14** Paza sauti kwa shangwe,
Ee binti ya Sayuni!
Paza sauti kwa ushindi, Ee
Israeli!^h
Shangilia na kufurahi kwa
moyo wako wote, Ee bin-
ti ya Yerusalemu!ⁱ

- 15** Yehova ameondoa huku-
mu ulizokabili.^j
Amemfukuza adui yako.^k
Mfalme wa Israeli,
Yehova, yuko katikati
yako.^l
Hutaogopa msiba tena.^m

SURA YA 3

a Isa 60:4

b Isa 45:17
Isa 54:4

c Isa 11:9

d Isa 57:15
Isa 61:1

e Isa 10:22
Mik 4:7

f Isa 60:21

g Yer 30:10
Eze 34:28
Eze 39:25, 26
Ho 2:18
Mik 4:4

h Ezr 3:11
Isa 12:5, 6
Zek 2:10

i Mik 4:8

j Isa 40:2
Zek 8:13

k Mik 7:10
Zek 2:8, 9

l Eze 48:35

m Amo 9:15
Zek 14:11

Safu ya 2

a Yer 46:28

b Isa 12:6

c Kum 30:9
Zb 147:11
Isa 62:3
Isa 65:19
Yer 32:41

d Omb 1:4
Omb 2:6

e Omb 5:1

f Isa 60:14
Zek 14:3

g Mik 4:6, 7

h Isa 11:11, 12
Isa 27:12
Eze 28:25
Eze 34:15, 16
Amo 9:14

i Isa 60:15

j Isa 61:7
Yer 30:10
Yer 33:7, 9
Eze 39:25, 27

- 16** Siku hiyo jiji la Yerusale-
mu litaambiwa:

“Usiogope, Ee Sayuni.^a
Usilegeze mikono yako.

- 17** Yehova Mungu wako yuko
katikati yako.^b

Akiwa Mwenye nguvu,
ataokoa.

Atakushangilia kwa sha-
ngwe kubwa.^c

Atakaa kimya* katika upe-
ndo wake.

Atakushangilia kwa kelele
za shangwe.

- 18** Nitawakusanya pamoja
wale wanaohuzunika
kwa sababu ya kukosa
sherehe zako;^d

Hawakuwa pamoja nawe
kwa sababu ya kubeba
shutuma yake.^e

- 19** Tazama! Wakati huo
nitawachukulia hatua
wote wanaokukanda-
miza;^f

Nami nitamwokoia yule
anayechechemea,^g

Nitawakusanya pamoja
waliotawanyika.^h

Nitawafanya kuwa kitu cha
sifa na umaarufu*

Katika kila nchi ambamo
waliaibishwa.

- 20** Wakati huo nitawaleta
ndani,

Wakati nitakapowakusa-
nya pamoja.

Kwa maana nitawafanya
kuwa kitu cha umaarufu*
na sifaⁱ miongoni mwa
mataifa yote duniani,
Nitakapowakusanya
mateka wenu mbele
ya macho yenu,^j
asema Yehova.^j

3:17 *Au “Atanyamaza; Atatulia; Atari-
dhika.” 3:19, 20 *Tnn., “jina.”

3:13 *Au “Watajilisha malishoni.”

HAGAI

YALIYOMO

- 1 Wakemewa kwa kutojenga hekalu (1-11)
'Je, ni wakati wa kukaa katika nyumba zilizopambwa kwa mbao?' (4)
"Kazienu mioyo yenu juu ya njia zenu" (5)
Kupanda kwa wingi kuvuna kidogo (6)
Watu wasikiliza sauti ya Yehova (12-15)
- 2 Hekalu la pili kujaa utukufu (1-9)

- Kutikiswa kwa mataifa yote (7)
Kukusanywa kwa vitu vyenye thamani vya mataifa (7)
Kujenga upya hekalu kwaleta baraka (10-19)
Utakatifu hauwezi kupitishwa kwa mwingine (10-14)
Ujumbe kwa Zerubabeli (20-23)
"Nitakufanya kuwa kama pete ya muhuri" (23)

1 Katika mwaka wa pili wa utawala wa Mfalme Dario, katika mwezi wa sita, siku ya kwanza ya mwezi huo, neno la Yehova lilikuja kupitia nabii Hagai^a kwa Zerubabeli^b mwana wa Shealtieli, gavana wa Yuda, na kwa YOSHUA mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu, likisema:

2 "Yehova wa majeshi anasema hivi: 'Watu hawa wanasema, "Wakati wa kujenga nyumba ya* Yehova bado haujafika."'"^c

3 Na neno la Yehova likaja tena kupitia nabii Hagai,^d likisema: **4** "Je, ni wakati wa ninyi kukaa katika nyumba zilizopambwa kwa mbao, huku nyumba hii ikiwa magofu?^e **5** Sasa hivi ndivyo anavyosema Yehova wa majeshi, 'Kazienu mioyo yenu juu ya* njia zenu. **6** Mmepanda mbegu nyingi, lakini mnavuna kidogo.^f Mnakula, lakini hamshibi. Mnakunywa, lakini hamto-sheki. Mnavaa nguo, lakini hakuna yeyote anayepata joto.

1:1 *Maana yake "Aliyezaliwa Wakati wa Serehe." 1:2 *Au "kujenga upya hekalu la." 1:5, 7 *Au "Fikirieni kwa makini."

SURA YA 1

a Ezr 5:1

b Ezr 3:2
Ezr 5:2

c Ezr 4:4, 23

d Ezr 6:14

e Yer 52:12, 13

f Kum 28:22

Safu ya 2

a Ezr 3:7

b Ezr 5:2
Ezr 6:15
Zek 1:16

c Isa 60:13

d Mal 2:2

e Hag 1:4

f Mt 1:12

g 1Nya 3:17-19
Lu 3:23, 27

h 1Nya 6:15

Kibarua huweka mshahara wake katika mfuko uliojaa mashimo."

7 "Yehova wa majeshi anasema hivi: 'Kazienu mioyo yenu juu ya* njia zenu.'

8 "'Pandeni juu mlimani mkalete miti.^a Jengeni nyumba hii,^b ili niifurahie na ili nitukuzwe,"^c asema Yehova."

9 "'Mitazamia mavuno mengi lakini mlipata kidogo; na mlipoyaleta katika nyumba hii, niliyapeperusha mbali.^d Kwa nini?' auliza Yehova wa majeshi. 'Kwa sababu nyumba yangu ni magofu, huku kila mmoja wenu akikimbia huku na huku ili kuitanza nyumba yake mwenyewe.^e **10** Kwa hiyo mbingu zilizo juu yenu zikazuia umande wake, na dunia ikazuia mazao yake. **11** Nami niliendelea kuuita ukame uje duniani, milimani, kwenye nafaka, kwenye divai mpya, kwenye mafuta, kwenye mimea inayoota ardhini, juu ya wadamu na mifugo, na juu ya kazi yote ya mikonu yenu.'"

12 Zerubabeli^f mwana wa Shealtieli^g na YOSHUA mwana wa Yehosadaki,^h kuhani

mkuu, na watu wengine wote wakaisikiliza sauti ya Yehova Mungu wao na maneno ya nabii Hagai, kwa sababu Yehova Mungu wao alikuwa ametuma; na watu wakaanza kuogopa kwa sababu ya Yehova.

13 Kisha Hagai, mjumbe wa Yehova, akawapa watu ujumbe huu kulingana na utume wake kutoka kwa Yehova: “Niko pamoja nanyi,^a asema Yehova.”

14 Basi Yehova akaichochea roho^b ya Zerubabeli mwana wa Shealtieli, gavana wa Yuda,^c na roho ya Yohshua^d mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu, na roho ya watu wengine wote; nao wakaja na kuanza kujenga nyumba ya Yehova wa majeshi, Mungu wao.^e **15** Ilikuwa siku ya 24 ya mwezi wa sita, katika mwaka wa pili wa Mfalme Dario.^f

2 Katika mwezi wa saba, siku ya 21 ya mwezi huo, neno la Yehova lilikuja kupitia nabii Hagai,^g likisema: **2** “Tafadhali muulize hivi Zerubabeli^h mwana wa Shealtieli, gavana wa Yuda,ⁱ na Yohshua^j mwana wa Yehosadaki,^k kuhani mkuu, na watu wengine wote: **3** ‘Ni nani aliyebaki miongoni mweni ambaye aliiona nyumba hii* katika utukufu wake wa mwanzoni?’^l Sasa mnaionaje? Je, hamwoni kwamba ni duni ikilinganishwa na ilivyokuwa?’^m

4 “Lakini sasa jipe moyo Zerubabeli,ⁿ asema Yehova, ‘jipe moyo Yohshua mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu.’

“Nanyi watu wote wa nchi, jipeni moyo,^o asema Yehova, ‘na mfanye kazi.’

“Kwa maana niko pamoja nanyi,^p asema Yehova wa ma-

2:3 *Au “hekalu hili.”

SURA YA 1

a 2Nya 15:2
Isa 8:10
Ro 8:31

b Ezr 1:1, 5

c Ezr 1:8
Ezr 5:14

d Zek 3:1
Zek 6:11-13

e Ezr 5:2
Zek 6:15

f Ezr 4:24
Hag 1:1
Zek 1:1

SURA YA 2

g Ezr 5:1
Ezr 6:14

h 1Nya 3:17-19
Zek 4:9

i Ezr 1:8

j Zek 3:8
Zek 6:11

k 1Nya 6:15

l 1Fa 6:1
Ezr 3:12

m Zek 4:10

n Zek 8:9

o Kut 3:12
Isa 43:2
Ro 8:31

Safu ya 2

a Kut 29:45
Kut 34:10

b Zek 4:6

c Isa 41:10
Zek 8:13

d Ebr 12:26, 27

e Isa 2:2
Isa 60:5, 11

f Kut 40:35
1Fa 8:11
Isa 66:12

g Isa 60:13

h Zb 85:8
Isa 2:4
Isa 60:17, 18
Zek 8:12

i Hag 1:1

j Mal 2:7

jeshi. **5** ‘Kumbukeni ahadi niliyowapa mlipotoka Misri,^a na roho yangu bado imo miongoni mweni.’^b Msiogope.”^c

6 “Kwa maana Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Kwa mara nyingine tena—baada ya muda mfupi—nitatikisa mbingu na dunia na bahari na nchi kavu.’^d

7 “Nami nitayatikisa mataifa yote, na vitu vyenye thamani* vya mataifa yote vitaingia katika nyumba hii;^e nami nitajaza nyumba hii utukufu,^f asema Yehova wa majeshi.

8 “‘Fedha ni yangu, na dhahabu ni yangu,’ asema Yehova wa majeshi.

9 “‘Utukufu wa wakati ujao wa nyumba hii utakuwa mkubwa zaidi kuliko ule wa mwanzoni,’ asema Yehova wa majeshi.

“Na mahali hapa nitawapa amani,^h asema Yehova wa majeshi.”

10 Katika siku ya 24 ya mwezi wa 9, mwaka wa pili wa utawala wa Dario, neno la Yehova lilimjia nabii Hagai,ⁱ likisema: **11** “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Tafadhali, waulize hivi makuhani kuhusu sheria.’^j **12** “Mtu akibeba nyama takatifu ndani ya upindo wa vazi lake, na vazi lake liguse mkate au mchuzi au divai au mafuta au chakula cha aina yoyote, je, kitakuwa kitakatifu?”^k

Makuhani wakajibu: “Hapana!”

13 Kisha Hagai akawauliza: “Mtu asiye safi kwa sababu ya kugusa maiti,* akigusa

2:5 *Au labda, “na roho yangu ilipokuwa ikisimama miongoni mweni.” 2:7 *Au “kutamanika.” 2:13 *Au “nafsi iliyokuwa.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

chochote kati ya vitu hivyo, je, kitu hicho kitakuwa kichafu?”^a

Makuhani wakajibu: “Kitakuwa kichafu.”

14 Basi Hagai akasema: “Hivyo ndivyo watu hawa walivyo, na hivyo ndivyo taifa hili lilivyo mbele zangu,’ asema Yehova, ‘na hivyo ndivyo kazi yote ya mikono yao ilivyo; chochote wanachotoa huko ni kichafu.’

15 “Lakini sasa, tafadhali, kazeni moyo wenu juu ya* jambo hili kuanzia leo na kuanzia leo na kuanzia leo na kuanzia leo: Kabla jiwe halijawekwa juu ya jiwe katika hekalu la Yehova,^b **16** hali ilikuwaje wakati huo? Mtu alipoenda kwenye rundo la nafaka akitarajia kupata vipimo 20, alipata vipimo 10 tu; na mtu alipoenda kwenye mtungi wa kushinikizia divai kuchota vipimo 50 kutoka kwenye pipa la divai, alipata vipimo 20 tu;^c **17** niliwapiga ninyi—kazi zote za mikono yenu—kwa upepo unaochoma na kuvu^d na mvua ya mawe, lakini hakuna hata mmoja wenu aliyenirudia,’ asema Yehova.

18 “Tafadhali, kazeni moyo wenu juu ya* jambo hili kua-

2:15, 18 *Au “fikirieni kwa makini.”

SURA YA 2

a Law 7:21
Hes 5:2, 3
Hes 9:6
Hes 19:11
Hes 31:19

b Ezr 3:10
Zek 4:9

c Hag 1:6
Zek 8:10

d Kum 28:22

Safu ya 2

a Ezr 5:2
Zek 8:9

b Hag 1:6

c Met 3:9, 10
Zek 8:12

d Hag 2:10

e Hag 2:6
Ebr 12:26, 27

f Isa 60:12
Da 2:44
Sef 3:8

g Amu 7:22

h Ezr 3:8

i Mt 1:12

nzia leo na kuanzia leo, kuanzia siku ya 24 ya mwezi wa 9, kuanzia siku ambayo msingi wa hekalu la Yehova uliwekwa;^a kazeni moyo wenu juu ya jambo hili: **19** Je, bado kuna mbegu katika ghala?^{* b} Mzabibu, mtini, mkomamanga, na mzeituni—haijazaa matunda, au je, imezaa? Kuanzia leo nitawaletea baraka.”^c

20 Neno la Yehova likamjia Hagai mara ya pili katika siku ya 24 ya mwezi huo,^d likisema: **21** “Mwambie Zerubabeli, gavana wa Yuda, ‘Nitazitikisa mbingu na dunia.’ **22** Nitapindua kiti cha ufalme cha falme na kuharibu kabisa nguvu za falme za mataifa;^e nami nitayapindua magari ya vita na wale wanaoenda, ^g na farasi na wapanda farasi watauawa, kila mmoja kwa upanga wa ndugu yake.”

23 “‘Siku hiyo,’ asema Yehova wa majeshi, ‘nitakuchukua, mtumishi wangu Zerubabeli^h mwana wa Shealtieli,’ⁱ asema Yehova, ‘nitakufanya kuwa kama pete ya muhuri, kwa sababu nimekuchagua wewe,’ asema Yehova wa majeshi.”

2:19 *Au “shimo la nafaka?”

ZEKARIA

YALIYOMO

- 1 Mwito wa kumrudia Yehova (1-6)
‘Nirudieni nami nitawarudia’ (3)
Maono ya 1: Wapanda farasi katikati ya mihadasi (7-17)
‘Yehova atalifariji tena Sayuni’ (17)
Maono ya 2: Pembe nne na mafundi wanne (18-21)

- 2 Maono ya 3: Mtu mwenye kamba ya kupimia (1-13)
Yerusalemu litapimwa (2)
Yehova, “ukuta wa moto kulizunguka pande zote” (5)
Kugusa mboni ya jicho la Mungu (8)

- Watu wa mataifa mengi watajiunga na Yehova (11)
- 3 Maono ya 4: Kuhani mkuu avishwa mavazi mengine (1-10)
Shetani ampinga Kuhani Mkuu YOSHUA (1)
'Nitamleta mtumishi wangu anayeitwa Chipukizi!' (8)
- 4 Maono ya 5: Kinara cha taa na mizeituni miwili (1-14)
"Si kwa nguvu, bali kwa roho yangu" (6)
Usidharau siku inayoanza kwa mambo madogo (10)
- 5 Maono ya 6: Kitabu cha kukunjwa kinachopaa angani (1-4)
Maono ya 7: Kikapu cha kupimia (5-11)
Kina mwanamke anayefaninisha Uovu (8)
Kikapu hicho chapelekwa Shinari (9-11)
- 6 Maono ya 8: Magari manne (1-8)
Chipukizi atakuwa mfalme na kuhani (9-15)
- 7 Yehova awashutumu wanaofunga kwa unafiki (1-14)
"Je, kweli mlifunga kwa ajili yangu?" (5)
'Mtendeane kwa haki, upendo mshikamanifu, na huruma' (9)
- 8 Yehova aleta amani na ukweli Sayuni (1-23)
Yerusalemu, "jiji la ukweli" (3)
"Kila mtu amwambie mwenzake ukweli" (16)
Siku za kufunga zitakuwa siku za sherehe (18, 19)
'Twendeni kwa bidii kumtafuta Yehova' (21)
- Watu kumi watahika joho la Myahudi (23)
- 9 Mungu ayahukumu mataifa jirani (1-8)
Kuja kwa mfalme wa Sayuni (9, 10)
Mfalme mnyenyekevu apanda juu ya punda (9)
Watu wa Yehova watawekwa huru (11-17)
- 10 Mwombeni Yehova awape mvua, msiombe miungu ya uwongo (1, 2)
Yehova awaunganisha watu wake (3-12)
Kiongozi kutoka katika nyumba ya Yuda (3, 4)
- 11 Madhara ya kumkataa mchungaji wa kweli aliyetumwa na Mungu (1-17)
"Lichunge kundi la kondoo wanaopaswa kuchinjwa" (4)
Fimbo mbili: Uzuri na Muungano (7)
Mshahara wa mchungaji: vipande 30 vya fedha (12)
Fedha hizo zatupwa kwenye hazina (13)
- 12 Yehova atalinda Yuda na Yerusalemu (1-9)
Yerusalemu, "jiwe zito" (3)
Wamlilia waliyemdunga (10-14)
- 13 Sanamu na manabii wa uwongo waondolewa (1-6)
Manabii wa uwongo wataaibika (4-6)
Mchungaji atapigwa (7-9)
Theluthi ya watu kusafishwa (9)
- 14 Ibada ya kweli yashinda kabisa (1-21)
Mlima wa Mizeituni utagawanyika katikati (4)
Yehova atakuwa Mungu pekee, na jina lake litakuwa ndilo jina pekee (9)
Ugonjwa utakaowapata wanaopigana na Yerusalemu (12-15)
Sherehe ya Vibanda (16-19)
Kila chungu kitakuwa kitakatifu kwa Yehova (20, 21)

1 Katika mwezi wa nane, mwaka wa pili wa utawala wa Darío,^a neno la Yehova lilimjia nabii Zekaria^{*b} mwa-

1:1 *Maana yake "Yehova Ameku- mbuka."

SURA YA 1

^a Ezr 4:24

Hag 1:1

Hag 2:10

^b Ezr 5:1

Safu ya 2

^a 2Fa 22:16, 17

Yer 44:5, 6

na wa Berekia mwana wa Ido, likisema: **2** "Yehova aliwaka-sirikia vikali baba zenu.^a

3 "Waambie, 'Yehova wa majeshi anasema hivi: "Niru-dieni,' asema Yehova wa majeshi, 'nami nitawarudia

ninyi,^a asema Yehova wa majeshi.”

4 “Msiwe kama baba zenu walioambiwa hivi na manabii wa kale: “Yehova wa majeshi anasema, ‘Tafadhali, geukeni* kutoka katika njia zenu ovu na matendo yenu maovu.’”^b

“Lakini hawakusikiliza, wala hawakunikazia uangali-fu,^c asema Yehova.

5 “Baba zenu wako wapi sasa? Na je, manabii wanai-shi milele? **6** Hata hivyo, je, maneno yangu na maagizo yan-gu niliyowaamuru watumishi wangu, manabii, hayakutimia kwa baba zenu?”^d Basi wakani-rudia na kusema: ‘Yehova wa majeshi ametutenda kulinga-na na njia zetu na matendo yetu, kama alivyokusudia ku-tutenda.’”^e

7 Katika siku ya 24 ya mwe-zi wa 11, yaani, mwezi wa She-bati,* katika mwaka wa pili wa utawala wa Dario,^f neno la Yehova lilimjia nabii Zeka-ria mwana wa Berekia mwana wa Ido, likisema: **8** “Niliona maono wakati wa usiku. Nili-mwona mtu akiendesha farasi mwekundu, akasimama tuli bondeni katikati ya miti ya mi-hadasi; na nyuma yake kuliku-wa na farasi wekundu, wa ka-hawia, na weupe.”

9 Basi nikauliza: “Hawa ni nani, bwana wangu?”

Malaika aliyekuwa akizu-ngumza nami akanijibu: “Nita-kuonyesha hawa ni nani.”

10 Kisha mtu huyo aliye-simama tuli katikati ya mi-hadasi akasema: “Hawa ndio wale ambao Yehova amewatu-ma watembe huku na huku

1:4 *Au “rudini.” 1:7 *Angalia Nyonge-za B15.

SURA YA 1

a Eze 33:11
Mik 7:18, 19
Mal 3:7

b Eze 9:6, 7
Isa 1:16
Isa 55:7
Ho 14:1

c 2Nya 36:15, 16
Yer 11:7, 8

d 2Nya 36:17
Da 9:11, 12

e Kum 28:20, 45
Yer 23:20

f Eze 4:24

Safu ya 2

a Zek 1:15

b Zb 74:10
Zb 102:13

c 2Nya 36:20, 21
Yer 25:11, 12
Da 9:2
Zek 7:5

d Yoe 2:18
Zek 8:2

e Yer 48:11
Zek 1:11

f Isa 54:8

g Zb 137:7
Isa 47:6
Yer 51:35

h Isa 12:1
Yer 33:14
Zek 8:3

i Eze 6:14, 15
Isa 44:28
Hag 1:14

j Yer 31:38, 39
Eze 40:2, 3
Zek 2:1, 2

k Isa 51:3

l Zb 132:13
Zek 2:12
Zek 3:2

m Zek 1:21

duniani.” **11** Nao wakamwa-mbia malaika huyo wa Yeho-va aliyekuwa amesimama ka-tikati ya mihadasi: “Tumete-mbea huku na huku duniani, na tazama! dunia yote imetu-lia na haina vurugu.”^a

12 Basi malaika wa Yehova akauliza: “Ee Yehova wa ma-jeshi, utaendelea hadi lini ku-kataa kuwaonyesha rehema wakaaji wa Yerusalemu na wa majiji ya Yuda,^b ambao umewa-kasirikia kwa miaka hii 70?”^c

13 Yehova akamjibu kwa maneno ya fadhili na ye-nye kufariji malaika huyo ali-yekuwa akizungumza nami.

14 Kisha malaika huyo aliye-kuwa akizungumza nami aka-niambia: “Tangaza hivi kwa sauti, ‘Yehova wa majeshi anasema hivi: “Nina bidii kwa ajili ya Yerusalemu na Sayuni, bidii nyingi.”^d **15** Kwa ha-sira kali nimeyakasirikia ma-taifa yanayostarehe,^e kwa sa-babu niliwakasirikia kidogo watu wangu,^f lakini yalizidi-sha msiba wao.”^g

16 “Basi Yehova anasema hivi: “Nitarudi Yerusalemu kwa rehema,^h na nyumba yan-gu mwenyewe itajengwa humo,”ⁱ asema Yehova wa majeshi, “na kamba ya kupi-mia itanyoosha juu ya Yeru-salemu.”^j

17 “Tangaza tena hivi kwa sauti: ‘Yehova wa majeshi anasema, “Majiji yangu yata-furika wema tena; na Yehova atalifariji tena Sayuni^k na ku-lichagua tena Yerusalemu.””^l

18 Kisha nikatazama juu na kuona pembe nne.^m **19** Kwa hiyo nikamuuliza malaika ali-yekuwa akizungumza nami: “Pembe hizi zinamaanisha nini?” Akanijibu: “Pembe hizi

ndizo zilizowatawanya watu wa Yuda,^a Israeli,^b na Yerusalemu.”^c

20 Kisha Yehova akanionyesha mafundi wanne. **21** Nikauliza: “Hawa wanakuja kufanya nini?”

Akakajibu: “Hizi ndizo pembe zilizowatawanya watu wa Yuda hivi kwamba hakuna yeyote aliyeweza kuinua kichwa chake. Mafundi hawa watakuja kuzitisha, kuziangusha chini pembe za mataifa yaliyoinua pembe zao dhidi ya nchi ya Yuda, ili kuwatawanya wakaaji wake.”

2 Nami nikatazama juu na kumwona mtu akiwa na kamba ya kupimia^d mkononi mwake. **2** Kwa hiyo nikaumuliza: “Unaenda wapi?”

Akanijibu: “Naenda kupima jiji la Yerusalemu, ili nijue upana wake na urefu wake.”^e

3 Na tazama! malaika aliyekuwa akizungumza nami akaondoka, na malaika mwingine akaja kukutana naye. **4** Kisha akamwambia: “Kimbia ukamwambie yule kijana, ‘‘Yerusalemu litakaliwa^f kama eneo la mashambani lililo wazi,* kwa sababu ya watu wengi na mifugo mingi iliyomo.’’^g **5** Nitakuwa ukuta wa moto kulizunguka pande zote,’’^h asema Yehova, “nami nitakuwa utukufu ndani yake.’’^h”ⁱ

6 “Njoo! Njoo! Kimbieni kutoka nchi ya kaskazini,’’^j asema Yehova.

“Kwa maana nimewatawanya kuelekea pepo nne za mbinguni,’’^k asema Yehova.

7 “Njoo, Ee Sayuni! Kimbia,

2:4 *Yaani, ambalo halijazingirwa na kuta. 2:6 *Tnn., “kwenye pande nne za mbinguni.”

SURA YA 1

a 2Fa 24:12, 14

b 2Fa 15:29

2Fa 17:6

2Fa 18:11

Yer 50:17

c 2Fa 25:11

2Nya 36:17, 19

SURA YA 2

d Zek 1:16

e Yer 31:38, 39

f Isa 44:26

Yer 30:18

Eze 36:10

g Isa 33:20

Yer 31:24

Yer 33:10, 11

Zek 8:4, 5

h Zb 125:2

Isa 26:1

i Isa 12:6

Isa 60:19, 20

Hag 2:9

j Isa 11:12, 16

k Kum 28:64

Eze 5:12

Safu ya 2

a Isa 48:20

Isa 52:2

Yer 50:8

Mik 4:10

b 2Fa 24:2

Mik 4:11

c Kum 32:9, 10

Zb 105:14, 15

2Th 1:6

d Isa 14:2

e Isa 35:10

f Isa 40:9, 10

g Law 26:11, 12

Isa 12:6

h Zb 22:27

Isa 2:2, 3

Zek 8:22, 23

i 2Nya 6:6

Zek 1:17

SURA YA 3

j Ezr 5:2

Hag 1:14

Zek 6:11

k Ayu 1:6

l Yud 9

m 2Nya 6:6

Zek 2:12

wewe unayekaa na binti ya Babiloni.^a **8** Kwa maana hivi ndivyo anavyosema Yehova wa majeshi, ambaye baada ya kutukuzwa* amenituma kwa mataifa yaliyokuwa yakiwapora ninyi:^b ‘‘Yeyote anayewagusa ninyi anaigusa mboni ya jicho langu.’’^c **9** Kwa maana sasa nitaupunga mkono wangu dhidi yao, nao watakuwa nyara kwa watumwa wao wenyewe.’^d Na hakika mtajua kwamba Yehova wa majeshi amenituma.

10 ‘‘Paza sauti kwa shangwe, Ee binti ya Sayuni;^e kwa maana ninakuja,^f nami nita-kaa kati yako,’’^g asema Yehova. **11** ‘‘Mataifa mengi yatajiunga na Yehova siku hiyo,^h nao watakuwa watu wangu; nami nitakaa kati yenu.’’ Nanyi mtalazimika kujua kwamba Yehova wa majeshi amenituma kwenu. **12** Yehova atamiliki Yuda kama fungu lake katika ardhi takatifu, naye atalichagua tena jiji la Yerusalemu.ⁱ **13** Nyamazeni, enyi nyote wenye mwili,* mbele za Yehova, kwa maana anachukua hatua kutoka kati-ka makao yake matakatifu.

3 Naye akanionyesha kuhani mkuu Yoshua^j akiwa amesimama mbele ya malaika wa Yehova, na Shetani^k alikuwa amesimama kwenye mkono wa kulia wa Yehova ili kumpinga. **2** Kisha malaika wa Yehova akamwambia Shetani: ‘‘Yehova na akukemee, ewe Shetani,^l naam, Yehova, ambaye amechagua Yerusalemu,^m na akukemee! Je, mtu huyu si gogo lililochomolewa motoni?’’

2:8 *Tnn., ‘‘baada ya utukufu.’’ ^aAu ‘‘analigusa jicho langu.’’ 2:13 *Au ‘‘wanadamu.’’

3 Sasa Yoshua alikuwa amevaa mavazi machafu akiwa amesimama mbele ya malaika.

4 Malaika akawaambia wale waliokuwa wamesimama mbele yake, "Mvueni mavazi yake machafu." Kisha akamwambia Yoshua, "Tazama! Nimefuta kosa lako,* nawe utavishwa mavazi bora."^{#a}

5 Basi nikasema: "Na avi-kwe kilemba safi kichwani."^b Nao wakamvika kilemba safi kichwani na kumvisha mavazi; na malaika wa Yehova alikuwa amesimama karibu.

6 Kisha malaika wa Yehova akamwambia Yoshua: 7 "Yehova wa majeshi anasema hivi, 'Ikiwa utatembea katika njia zangu na kutekeleza majukumu niliyokupa, utakuwa mwamuzi nyumbani mwangu^c na kuzitunza* nyua zangu; nami nitakuruhusu ufike mbele zangu, pamoja na hawa wanaosimama hapa.'

8 "Tafadhali sikiliza, Ee Kuhani Mkuu Yoshua, wewe pamoja na wenzako wanaoketi mbele yako, kwa maana wanaume hawa ni ishara; tazama! ninamleta mtumishi wangu^d anayeitwa Chipukizi!^e 9 Tazama jiwe ambalo nime-weka mbele ya Yoshua! Jiwe hili moja lina macho saba; nami ninachonga maandishi juu yake,^f asema Yehova wa majeshi, 'nami nitaondoa hatia ya nchi hiyo kwa siku moja.'^f

10 "Siku hiyo,^f asema Yehova wa majeshi, 'kila mmoja wenu atamwalika jirani yake aje chini ya mzabibu wake na chini ya mtini wake.'^g

3:4 *Au "hatia yako." [#]Au "majoho ya kifahari." 3:7 *Au "kusimamia; kulinda."

SURA YA 3

a Kut 28:2

b Kut 29:6

c Mal 2:7

d Isa 42:1
Isa 52:13e Isa 11:1
Isa 53:2, 11
Yer 23:5
Yer 33:15
Zek 6:12

f Yer 50:20

g 1Fa 4:25
Ho 2:18
Mik 4:4

Safu ya 2

SURA YA 4

a Kut 25:31
1Fa 7:48, 49

b Kut 25:37

c Zek 4:11, 14
Ufu 11:3, 4d 1Sa 17:45
Ho 1:7e Amu 6:34
Amu 15:14f Ezr 3:2
Hag 1:1

g Isa 40:4

h Ezr 3:8, 10
Ezr 5:14, 16i Ezr 6:14
Zek 6:12j Ezr 3:12
Hag 2:3

4 Malaika aliyekuwa akizungumza nami akarudi na kuniamsha, kama mtu anavyoamshwa kutoka usingizini.

2 Kisha akaniuliza: "Unaona nini?"

Nikamjibu: "Tazama! ninao-na kinara cha taa cha dhahabu tupu,^a na juu yake kuna bakuli. Kina taa saba juu yake,^b naam, saba, na taa hizo zilizo juu yake zina mirija saba.

3 Na kando yake kuna mizeituni miwili,^c mmoja upande wa kulia wa bakuli na mwingine upande wa kushoto."

4 Kisha nikamuuliza malaika aliyekuwa akizungumza nami: "Bwana wangu, vitu hivi vinamaanisha nini?" 5 Kwa hiyo malaika aliyekuwa akizungumza nami akaniuliza: "Hujui maana ya vitu hivi?"

Nikamjibu: "Sijui, bwana wangu."

6 Ndipo akaniambia: "Hili ndilo neno la Yehova kwa Zerubabeli: "Si kwa jeshi, wala si kwa nguvu,^d bali kwa roho yangu,"^e asema Yehova wa majeshi. 7 Wewe ni nani, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli^f utakuwa nchi tamberare.*^g Naye ataleta nje jiwe la juu kabisa la hekalu huku watu wakishangilia: "Ni zuri ajabu! Ni zuri ajabu!"^h

8 Neno la Yehova likanijia tena, likisema: 9 "Mikono ya Zerubabeli imeweka msingi wa nyumba hii,^h na mikono yake mwenyewe itaikamilisha.ⁱ Nanyi mtalazimika kujua kwamba Yehova wa majeshi amenituma kwenu. 10 Kwa maana ni nani ameidharau siku inayoanza kwa mambo madogo?^j Kwa maana wa-

4:7 *Au "uwanda." 4:10 *Tnn., "vitu vidogo."

tashangilia na kuona timazi* mkononi mwa Zerubabeli. Na haya macho saba ni macho ya Yehova, ambayo yanazunguka duniani kote.”^a

11 Kisha nikamuuliza: “Mizeituni hii miwili iliyo upande wa kulia na wa kushoto wa kinara cha taa inamaanisha nini?”^b **12** Nikamuuliza mara ya pili: “Mafungu haya mawili ya matawi ya mizeituni* yanayomimina mafuta ya dhahabu kupitia mirija miwili ya dhahabu yanamaanisha nini?”

13 Basi akaniuliza: “Hujui maana ya vitu hivi?”

Nikamjibu: “Sijui, bwana wangu.”

14 Akasema: “Hawa ndio wale watiwa-mafuta wawili wanaosimama kando ya Bwana wa dunia yote.”^c

5 Nikatazama juu tena, nikaona kitabu cha kukunjwa kikipaa. **2** Akaniuliza: “Unaona nini?”

Nikamjibu: “Ninaona kitabu cha kukunjwa chenye urefu wa mikono 20* na upana wa mikono 10 kikipaa.”

3 Kisha akaniambia: “Hii ndiyo laana inayotoka kwenda juu ya dunia yote, kwa sababu kila mtu anayeiba,^d kama ilivyoandikwa upande mmoja, hajaadhibiwa; na kila mtu anayeapa kwa uwongo,^e kama ilivyoandikwa upande wa pili, hajaadhibiwa. **4** ‘Nimeituma laana hiyo,’ asema Yehova wa majeshi, ‘nayo itaingia kati-ka nyumba ya mwizi na ka-

4:10 *Tnn., “jiwe, mkebe.” **4:12** *Yaani, matawi yaliyojaa zeituni. **5:2** *Mkono mmoja ulilingana na sentimita 44.5 (inchi 17.5). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 4

a 2Nya 16:9
Met 15:3
Yer 16:17
Ufu 5:6

b Zek 4:2, 3

c Hag 2:4
Ufu 11:3, 4

SURA YA 5

d Kut 20:15

e Kut 20:7
Law 19:12

Safu ya 2

a Mwa 10:8, 10
Mwa 11:1, 2
Da 1:2

tika nyumba ya mtu anayea-
pa kwa uwongo katika jina lan-
gu; nayo itakaa katika nyu-
mba hiyo na kuiharibu kabisa
na pia mbao zake na mawe
yake.”

5 Ndipo malaika aliyekuwa akizungumza nami akaja na kuniambia: “Tafadhali, tazama juu, uone kitu kinachotoka.”

6 Kwa hiyo nikamuuliza: “Ni kitu gani hicho?”

Akanijibu: “Ni chombo cha efa kinachotoka.”* Kisha akaniambia: “Hivyo ndivyo wanaoonekana duniani kote.” **7** Nami nikaona kwamba kifuniko chake cha mwingo cha madini ya risasi kilikuwa kimeinuliwa, na kulikuwa na mwanamke aliyekuwa ameketi ndani ya chombo hicho. **8** Kwa hiyo malaika akasema: “Huu ni Uovu.” Kisha akamsukuma mwanamke huyo ndani ya chombo hicho cha efa na kukifunika kwa nguvu kwa kile kifuniko kizito cha madini ya risasi.

9 Halafu nikatazama juu na kuwaona wanawake wawili wakija, nao walikuwa wakipaa katika upepo. Walikuwa na mabawa kama ya korongo. Nao wakakiinua kile chombo na kuruka nacho kati ya dunia na mbingu. **10** Basi nikamuuliza malaika aliyekuwa akizungumza nami: “Wanaki-peleka wapi chombo cha efa?”

11 Akanijibu: “Katika nchi ya Shinari*^a ili wamjengee nyumba mwanamke huyo;

5:6 *Tnn., “Ni efa inayotoka.” Efa inatumiwa hapa kurejelea chombo au kapu kilichotumiwa kupima kipimo cha efa. Efa ya nafaka ilikuwa karibu kilogramu 13. Angalia Nyongeza B14. **5:11** *Yaani, Babilonia.

na itakapokuwa tayari, atawekwa humo mahali panapomfaa.”

6 Kisha nikatazama juu tena na kuona magari manne ya vita yakitoka katikati ya milima miwili, na milima hiyo ilikuwa ya shaba. **2** Gari la kwanza lilikokotwa na farasi wekundu, na gari la pili, farasi weusi.^a **3** Gari la tatu lilikokotwa na farasi weupe, na gari la nne, farasi wenye madoodoa na mabaka.^b

4 Nikamuuliza malaika aliyekuwa akizungumza nami: “Magari haya yanamaanisha nini bwana wangu?”

5 Malaika huyo akanijibu: “Hizi ni zile roho nne^c za mbinguni zinazotoka baada ya kusimama mbele ya Bwana wa dunia yote.^d **6** Gari linalokokotwa na farasi weusi linaenda katika nchi ya kaskazini,^e farasi weupe wanaenda kuvuka bahari; na wale wenye madoodoa wanaenda katika nchi ya kusini. **7** Na farasi wenye mabaka walitamani sana kwenda kutembea kotekote duniani.” Kisha akasema: “Nendeni, tembeeni kotekote duniani.” Nao wakaanza kutembea kotekote duniani.

8 Kisha akaniita kwa sauti na kuniambia: “Tazama, farasi wanaoenda katika nchi ya kaskazini wameifanya roho ya Yehova itulie katika nchi ya kaskazini.”

9 Neno la Yehova likanijia tena, likisema: **10** “Chukua vitu ambavyo Heldai, Tobaya, na Yedaya walileta kutoa kwa watu walio uhamishoni; na siku hiyo, ni lazima uende katika nyumba ya Yosia mwana wa Sefania ukiwa pamoja na watu hawa walio-

SURA YA 6

a Zek 6:6

b Zek 6:7

c Zb 104:4

d 2Nya 18:18

Ayu 1:6

Da 7:10

Lu 1:19

Ebr 1:7, 14

e Zek 2:6, 7

Safu ya 2

a Hag 1:1

Zek 3:3, 5

b Isa 11:1

Zek 3:8

c Zek 8:9

d Ebr 3:1

Ebr 4:14

Ebr 8:1

e Zek 6:10

SURA YA 7

f Ebr 6:14

Zek 1:1

toka Babiloni. **11** Unapaswa kuchukua fedha na dhahabu, utengeneze taji* na kumvika kichwani Yoshua^a mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu. **12** Nawe umwambie,

“Yehova wa majeshi anesema hivi: “Ndiye huyu wwanamume anayelitwa Chipukizi.^b Atachipuka kutoka mahali pake mwenyewe, naye atalijenga hekalu la Yehova.^c **13** Yeye ndiye atakayelijenga hekalu la Yehova, na ndiye atakayepokea utukufu. Ataketi kwenye kiti chake cha ufalme na kutawala, naye atakuwa pia kuhani kwenye kiti chake cha ufalme,^d na kutakuwa na mapatano ya amani kati ya hivyo viwili.* **14** Na taji hilo* litakuwa kumbukumbu^e kwa Helemu, Tobaya, Yedaya,^e na Heni mwana wa Sefania, katika hekalu la Yehova. **15** Na wale walio mbali sana watakuja na kushiriki katika ujenzi wa hekalu la Yehova.” Nanyi mtalazimika kujua kwamba Yehova wa majeshi amenituma kwenu. Na itakuwa hivyo—ikiwa hamtakosa kuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu.”

7 Na katika mwaka wa nne wa utawala wa Mfalme Dario, neno la Yehova lilimjia Zekaria^f siku ya nne ya mwezi wa tisa, yaani, mwezi wa Kislevu.* **2** Watu wa Betheli walituma Shareza na Regemeleki na wanaume wake ili wamwombe Yehova kibali,* **3** wawaulize hivi makuha-

6:11, 14 *Au “taji lenye utukufu.” **6:13** *Yaani, kati ya cheo chake akiwa mtawala na cheo chake akiwa kuhani. **6:14** *Au “ukumbusho.” **7:1** *Angalia Nyoingeza B15. **7:2** *Tnn., “wautulize uso wa Yehova.”

ni wa nyumba ya* Yehova wa majeshi na pia manabii: “Je, nilie katika mwezi wa tano^a na kujinyima chakula, kama vile ambavyo nimekuwa nikifanya kwa miaka mingi sana?”

4 Neno la Yehova wa majeshi likanijia tena, likisema: **5** “Waambie watu wote nchini na makuhani, ‘Mlipofunga na kulia kwa sauti katika mwezi wa tano na mwezi wa saba^b kwa miaka 70,^c je, kweli mli-funga kwa ajili yangu? **6** Na mlipokuwa mkila na kunywa, je, hamkuwa mkila na kunywa kwa ajili yenu wenyewe? **7** Je, hampaswi kutii maneno ambayo Yehova alitangaza kupitia manabii wa kale,^d wakati jiji la Yerusalemu na majiji yaliyolizunguka yalipokuwa na wakaaji na yalipokuwa na amani, na watu walipokaa Ngebu na Shefela?”

8 Neno la Yehova likanjia tena Zekaria, likisema: **9** “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Hukumuni kwa haki ya kweli,^e na mtendeane kwa upendo mshikamanifu^f na rehema. **10** Msimpunje mjané wala yatima,^g mgeni^h wala maskini;ⁱ na katika mioyo yenu msipangiane njama za kutendeana uovu.’ **11** Lakini waliendelea kukataa kusikiliza,^k wakageuza migongo yao kwa ukaidi,^l na kuziba masikio yao ili wasisikie.^m **12** Waliifanya mioyo yao iwe kama almasiⁿ nao walikataa kutii sheria^o na maneno ambayo Yehova wa majeshi aliwapa kwa roho yake kupitia manabii wa

7:3 *Au “hekalu la.” 7:10 *Tnn., “mtoto asiye na baba.” 7:12 *Au labda, “jiwe gumu,” kama vile jiwe la msasa. ^aAu “mafundisho.”

SURA YA 7

- a 2Fa 25:8-10
Yer 52:12-14
b Yer 41:1, 2
c Yer 25:11
Zek 1:12
d 2Nya 36:15
e Met 21:3
Yer 21:12
f Met 16:6
Ho 10:12
Mik 6:8
g Kut 22:22
Kum 24:17
Isa 1:17
h Kut 23:9
Mal 3:5
i Met 22:22
j Zek 8:17
k 2Nya 33:10
Yer 6:10
l Ne 9:29
m 2Fa 17:13, 14
Isa 6:10
Yer 25:7
n Eze 3:7

Safu ya 2

- a Ne 9:30
Mdo 7:51
b 2Nya 36:15, 16
Yer 21:5
c Isa 50:2
d Isa 1:15
Omb 3:44
e Kum 28:64
Yer 5:15
f Law 26:22, 33
2Nya 36:20, 21

SURA YA 8

- g Yoe 2:18
Zek 1:14
h Zek 1:16
i Isa 12:6
Yoe 3:17
Zek 2:11
Zek 8:8
j Isa 1:26
Isa 60:14
Yer 33:16
k Isa 2:2
Isa 11:9
Isa 66:20
Yer 31:23
l Isa 65:20
Yer 30:10
m Yer 30:19
Yer 31:4, 27
Zek 2:4

kale.^a Kwa hiyo Yehova wa majeshi akakasirika sana.”^b

13 “Kama vile ambavyo hawakunisikiliza nilipowaita,^c mimi pia sikuwasikiliza waliponiita,^d asema Yehova wa majeshi. **14** ‘Nami niliwatawanya kwa kimbunga kotekote katika mataifa yote ambayo hawakuyajua,^e na nchi ikaa chwa ukiwa nyuma yao, hivi kwamba hakuna yeyote aliyeingia wala kutoka;^f kwa maana waliabadili nchi yenye kutamnika ikawa kitu cha kutisha.”

8 Neno la Yehova wa majeshi lilinijia tena, likisema: **2** “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Nitakuwa na bidii kwa ajili ya Sayuni, bidii nyingi,^g na kwa hasira kali nitakuwa na bidii kwa ajili yake.”

3 “Yehova anasema hivi: ‘Nitarudi Sayuni^h na ku-kaa Yerusalemu;ⁱ na Yerusalemu litaitwa jiji la ukweli,^j na mlima wa Yehova wa majeshi utaitwa mlima mtakatifu.”^k

4 “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Wanaume wazee na wanawake wazee wataketi tena katika viwanja vya jiji la Yerusalemu, kila mmoja wao akiwa na mkongojo wake mkononi kwa sababu ya umri wake mkubwa.’^l **5** Na viwanja vya jiji vitajaa wavulana na wasichana wanaocheza.”^m

6 “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Ingawa jambo hilo huenda likaonekana kuwa gumu kwa watu wa taifa hili watakabaki siku hizo, je, linaweza kuwa gumu sana machoni pangu pia?’ asema Yehova wa majeshi.”

8:3 *Au “uaminifu.” 8:4 *Tnn., “kwa sababu ya wingi wa siku.”

7 “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Tazama, ninawao-koa watu wangu kutoka katika nchi ya mashariki na nchi ya magharibi.*^a 8 Nami nitawaleta ndani, nao wataishi Yerusalemu;^b watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao^c katika ukweli* na katika uadilifu.”

9 “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Mikono yenu na iwe na nguvu,*^d ninyi ambao sasa mnasikia maneno haya yanayotoka katika kinywa cha manabii,^e maneno yaleyale yaliyosemwa siku ambayo msingi wa nyumba ya Yehova wa majeshi uliwekwa ili hekalu lijengwe. 10 Kwa maana kabla ya wakati huo, mshahara haukulipwa kwa ajili ya mwanadamu wala kwa ajili ya mnyama;^f na haikuwa salama kuingia wala kutoka kwa sababu ya maadui, kwa maana nilisababisha uadui kati ya watu wote.’

11 “Lakini sasa sitawate-ndea watu waliobaki wa taifa hili kama nilivyowatendea zamani,^g asema Yehova wa majeshi. 12 ‘Kwa maana mbe-gu ya amani itapandwa; mza-bibu utazaa matzao yake na dunia itatoa mazao yake,^h na mbingu zitatoa umande wake; nami nitawapa watu waliobaki wa taifa hili vitu hivi vyote viwe urithi wao.ⁱ 13 Na kama nilivyokuwa kitu cha kulaa-niwa miongoni mwa mataifa,^j Ee nyumba ya Yuda na nyumba ya Israeli, vivyo hivyo nitawaoko, nanyi mtakuwa baraka.^k Msiogope! Mikono yenu na iwe na nguvu.’*^m

8:7 *Au “nchi ya mawio ya jua na nchi ya machweo ya jua.” 8:8 *Au “uaminifu.” 8:9, 13 *Au “Iweni jasiri.”

SURA YA 8

a Zb 107:2, 3

b Yer 3:17
Yoe 3:20
Amo 9:14c Law 26:12
Yer 30:22
Eze 11:20d Isa 35:4
Hag 2:4

e Ezz 5:1

f Hag 1:6

g Hag 2:19

h Law 26:4
Kum 28:4
Isa 30:23i Isa 35:10
Isa 61:7j Kum 28:37
Yer 42:18k Mwa 22:18
Isa 19:24, 25

l Isa 41:10

m Isa 35:4

Safu ya 2

a Yer 4:28
Eze 24:14b Yer 31:28
Yer 32:42c Isa 43:1
Sef 3:16d Law 19:11
Met 12:19
Efe 4:25

e Zek 7:9

f Zek 7:10

g Zek 5:4

h Met 6:16-19

i Yer 52:6, 7

j Yer 52:12-14

k 2Fa 25:25
Zek 7:5

l Yer 52:4

m Isa 35:10
Yer 31:12

n Yer 50:4, 5

14 “Kwa maana Yehova wa majeshi anasema hivi: “Kama nilivyokusudia kuwaletea msiba kwa sababu mababu zenu walinikasirisha,” asema Yehova wa majeshi, “nami sikughairi,^a 15 ndivyo nilivyokusudia sasa kulitendea mema jiji la Yerusalemu na nyumba ya Yuda.^b Msiogope!”^c

16 “‘Haya ndiyo mambo mnayopaswa kufanya: Kila mtu amwambie mwenzake ukweli,^d na hukumu mnazotoa katika malango yenu zinapaswa kutetea ukweli na amani.^e 17 Msipangiane njama za msiba mioyoni mwenu,^f nanyi msipende kiapo chochote cha uwongo;^g kwa maana hayo yote ni mambo ninayochukia,^h asema Yehova.”

18 Neno la Yehova wa majeshi lilinjia tena, likisema: 19 Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Mfungo wa mwezi wa nne,ⁱ mfungo wa mwezi wa tano,^j mfungo wa mwezi wa saba,^k na mfungo wa mwezi wa kumi^l zitakuwa pindi za shangwe na kushangilia kwa ajili ya nyumba ya Yuda—sherehe za kushangilia.^m Kwa hiyo pendeni ukweli na amani.’

20 “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Itatukia kwamba mataifa na wakaaji wa majiji mengi watakuja; 21 na wakaaji wa jiji moja wataenda kwa wakaaji wa jiji lingine na kuwaambia: “Twendeni kwa bidii tukamsihi Yehova atupe kibali chake* na kumtafuta Yehova wa majeshi. Mimi pia nitaenda.”ⁿ 22 Na mataifa mengi na mataifa yenye nguvu yatakuja Yerusalemu kumtafuta Yehova wa ma-

8:21 *Tnn., “tukautulize uso wa Yehova.”

jeshi^a na kumsihi Yehova awape kibali chake.’*
 23 “Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Siku hizo watu kumi kutoka katika lugha zote za mataifa^b watahika, naam, watahika kwa nguvu joho* la Myahudi,[#] wakisema: “Tunataka kwenda pamoja nanyi,^c kwa maana tumesikia kwamba Mungu yupo pamoja nanyi.””^d

9 Tangazo:

“Neno la Yehova liko dhidi ya nchi ya Hadraki, Nalo linalenga* Damasko^e —Kwa maana macho ya Yehova yanawaangalia wanadamu^f

Na makabila yote ya Israeli—

2 Na dhidi ya Hamathi,^g inayopakana nayo,

Na dhidi ya majiji ya Tiro^h na Sidoni,ⁱ kwa maana yana hekima nyingi.^j

3 Jiji la Tiro lilijengea boma.*

Lilirundika fedha kama mavumbi

Na dhahabu kama mavumbi barabarani.^k

4 Tazama! Yehova atachukua mali za jiji hilo, Naye ataliangamiza jeshi lake baharini,^l

Na jiji hilo litateketezwa motoni.^m

5 Jiji la Ashkeloni litaona jambo hilo na kuogopa; Gaza litahisi maumivu makali sana, Ekroni pia, kwa sababu tumaini lake limeaibishwa.

8:22 *Tnn., “kuutuliza uso wa Yehova.”
 8:23 *Au “upindo wa vazi.” #Tnn., “mwanamume Myahudi.” 9:1 *Tnn., “litapumzika.” 9:3 *Au “ngome.”

SURA YA 8

a Zb 22:27
 Isa 2:2, 3
 Isa 11:10
 Isa 55:5
 Isa 60:3
 Ho 1:10
 Mik 4:2
 Hag 2:7

b Zek 2:11
 Ufu 7:9
 Ufu 14:6

c Kut 12:37, 38

d Isa 45:14

SURA YA 9

e Yer 49:27
 Amo 1:3

f Ebr 4:13
 IPe 3:12

g Yer 49:23

h Isa 23:1
 Amo 1:9, 10

i Eze 28:21
 Yoe 3:4

j Eze 28:2, 3

k Eze 27:32, 33

l Eze 26:17
 Eze 27:26

m Eze 28:18

Safu ya 2

a Sef 2:4

b Amo 1:8

c Isa 60:14

d 2Sa 5:6, 7
 1Fa 9:20, 21

e Zb 125:2

f Isa 54:14

g Zb 2:6
 Isa 32:1
 Yer 23:5
 Lu 19:37, 38
 Yoh 1:49

h Mt 11:29

i 1Fa 1:33, 34
 Mt 21:5, 7
 Yoh 12:14, 15

Mfalme wa Gaza ataangamizwa,
 Na Ashkeloni halitakaliwa na watu.^a

6 Mwanaharamu ataishi Ashdodi,

Nami nitakikomesha kiburi cha Mfilisti.^b

7 Nitaondoa vitu vyenye damu kutoka kinywani mwake

Na vitu vyenye kuchukiza kutoka katikati ya meno yake,

Naye atabaki kwa ajili ya Mungu wetu;

Naye atakuwa kama shehe* nchini Yuda,^c

Na Ekroni kama Myebusi.^d

8 Nitapiga kambi nikiwa mlinzi wa nyumba yangu,^e

Hivi kwamba hakuna yeyote atakayeingia na hakuna yeyote atakayetoka;

Na hakuna msimamizi wa watumwa* atakayeingia humo tena,^f

Kwa maana sasa nimeyaoana[#] kwa macho yangu.

9 Shangilia sana, Ee binti ya Sayuni.

Paza sauti kwa ushindi, Ee binti ya Yerusalemu.

Tazama! Mfalme wako anakuja kwako.^g

Yeye ni mwadilifu, analeta wokovu,*

Ni mnyenyekevu^h na amepanda punda,

Amepanda mwanapunda dume,[#] mwana wa punda jike.ⁱ

9:7 *Shehe alikuwa mkuu wa kabilala. 9:8 *Au “mkandamizaji.” #Inaonekana ni mateso ya watu wake. 9:9 *Au “naye ni mshindi; na ameokolewa.” #Au “punda dume.”

- 10** Nitaondoa gari la vita
Efraimu
Na farasi kutoka Yerusa-
lemu.
Upinde wa vita utachuku-
liwa.
Naye atatangaza amani
kwa mataifa;^a
Utawala wake utaenea ku-
toka bahari mpaka
bahari
Na kutoka Mto Efrati mpa-
ka kwenye miisho ya
dunia.^b
- 11** Lakini wewe, Ee mwana-
mke, kwa damu ya agano
lako,
Nitawatoa wafungwa wako
katika shimo lisilo na
maji.^c
- 12** Rudini katika ngome,
enyi wafungwa wenye
tumaini.^d
Leo ninakwambia,
'Nitakulipa fungu maradu-
fu, ewe mwanamke.^e
- 13** Kwa maana nitampinda*
Yuda kama upinde
wangu.
Nitamjaza Efraimu kwenye
upinde,[#]
Nami nitawaamsha wana
wako, Ee Sayuni,
Dhidi ya wana wako, Ee
Ugiriki,
Nami nitakufanya uwe
kama upanga wa shujaa.^f
- 14** Itaonekana kwamba Yeho-
va yupo pamoja nao,
Na mshale wake utafyatu-
ka kama radi.
Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova atapiga pembe,^f
Naye atasonga mbele pa-
moja na dhoruba za upe-
po za kusini.

9:13 *Tnn., "nitamkanyaga." #Yaani, kama mshale.

SURA YA 9

a Isa 9:7

b Kut 23:31
Zb 2:8
Zb 72:8

c Isa 49:9

d Isa 61:1
Yer 31:17

e Isa 61:7

f Yos 6:5

Safu ya 2

a Mik 5:9
Zek 10:5
Zek 12:6b Kut 27:2
Law 4:7

c Eze 34:22

d Isa 62:3
Sef 3:20e Zb 25:8
Zb 31:19
Isa 63:7f Isa 62:8
Yoe 3:18
Amo 9:13

SURA YA 10

g Kum 11:14
Yer 14:22
Yer 51:16
Eze 34:26
Yoe 2:23

- 15** Yehova wa majeshi atawa-
linda,
Nao watayameza na kuya-
tiisha mawe ya kombeo.^a
Watakunywa na kupiga ke-
lele, kana kwamba wa-
mekunywa divai;
Nao watajazwa kama ba-
kuli,
Kama pembe za madha-
bahu.^b
- 16** Yehova Mungu wao ata-
waokoa siku hiyo
Wakiwa kundi la watu
wake;^c
Kwa maana watakuwa
kama vito vya taji vina-
vyong'aa kwenye ardhi
yake.^d
- 17** Jinsi wema wake ulivyo
mwingi kwelikweli,^e
Na jinsi uzuri wake una-
vyovutia ajabu!
Nafaka itawafanya vijana
wanaume wanawiri,
Na divai mpya itawafanya
mabikira wanawiri.^f
- 10** "Mwombeni Yehova
mvua wakati wa mvua
ya masika.
Yehova ndiye anayete-
ngeneza mawingu ya
dhoruba,
Ndiye anayewaletea mvua,^g
Na kumpa kila mtu mimea
ya shambani.
- 2** Kwa maana sanamu za te-
rafimu* zimesema uwo-
ngo;[#]
Na wabashiri^Δ wameona
maono ya uwongo.
Husimulia ndoto zisizo na
faida,
Na kwa ubatili wao hujari-
bu kufariji.

10:2 *Au "miungu ya familia; sanamu."
#Au "zimesema mambo ya uchawi; ma-
zingaombwe." ^ΔAu "waaguzi."

Ndiyo sababu watatanga-tanga kama kondoo.

Watateseka, kwa maana hakuna mchungaji.

- 3** Hasira yangu inawaka dhidi ya wachungaji, Nitawaadhibu viongozi* wanaowakandamiza watu;

Kwa maana Yehova wa majeshi amelielekezea uangalifu kundi lake,^a amelelekezea uangalifu nyumba ya Yuda,

Naye amewafanya wawe kama farasi wake mwenye fahari vitani.

- 4** Mtu mkuu anatoka kwake,* Mtawala anayemtegemeza anatoka kwake,[#]

Upinde wa vita unatoka kwake;

Na kila mwangalizi[^] hutoka kwake, wote pamoja.

- 5** Nao watakuwa kama mashujaa, Wanaokanyaga matope barabarani wakiwa vitani. Watapigana vita, kwa maana Yehova yupo pamoja nao;^b

Na wapanda farasi wataabishwa.^c

- 6** Nitaifanya nyumba ya Yuda iwe kuu sana, Nami nitaiokoa nyumba ya Yosefu.^d Nitawarudisha, Kwa maana nitawaonyesha rehema,^e

10:3 *Tnn., "mabeberu." **10:4** *Tnn., "Mnara wa pembeni unatoka kwake," unafananisha mtu muhimu au wa maana sana; kiongozi. [#]Tnn., "Kigingi kinatoka kwake," kinafananisha mtegemezaji; mtawala." [^]Au "msimamizi wa watumwa."

SURA YA 10

a Eze 34:16, 17

b Kum 20:1

c Hag 2:22

d Yer 3:18
Eze 37:16, 19
Ho 1:10, 11

e Yer 31:9, 20

Safu ya 2

a Yer 30:18

b Zek 9:15

c Isa 66:14
Sef 3:14

d Isa 44:22
Isa 51:11

e Isa 11:11

f Yer 50:19
Mik 7:14

g Isa 49:19, 20
Isa 54:1, 2

h Isa 11:15

i Isa 19:1
Eze 30:13

Nao watakuwa kama watu ambao sijawahi kuwataupa;^a

Kwa maana mimi ni Yehova Mungu wao, nami nitawajibu.

- 7** Ni lazima watu wa Efraimu wawe kama shujaa hodari,

Na moyo wao utashangilia kana kwamba wamekunywa divai.^b

Wana wao wataona jambo hilo na kushangilia;

Moyo wao utashangilia katika Yehova.^c

- 8** 'Nitawapigia mluzi na kuwakusanya pamoja; Kwa maana nitawakomboa,^d nao watakuwa wengi,

Na kuendelea kuongezeka.

- 9** Ingawa ninawatawanya kama mbegu miongoni mwa mataifa, Watanikumbuka wakiwa katika maeneo ya mbali; Watahuishwa na kurudi pamoja na wana wao.

- 10** Nitawarudisha kutoka nchini Misri

Na kuwakusanya kutoka Ashuru;^e

Nitawaleta katika nchi ya Gileadi^f na Lebanoni,

Na hakutakuwa na nafasi zaidi ya kuwatosha.^g

- 11** Ni lazima apite baharini kwa msukosuko;

Na humo baharini atayapiga mawimbi yatulie;^h

Vilindi vyote vya Mto Nile vitakauka.

Kiburi cha Ashuru kita-shushwa,

Na fimbo ya mfalme wa Misri itaondoka.ⁱ

12 Nitawafanya wawe wakuu sana katika jina langu Yehova,^a

Nao watatembea huku na kule katika jina langu,^b asema Yehova.”

11 “Fungua milango yako, Ee Lebanoni, Ili moto uteketeze mierezi yako.

2 Omboleza kwa sauti, ewe mberoshi, kwa maana mwerezi umeanguka; Miti mikubwa imeharibiwa! Ombolezeni kwa sauti, enyi mialoni ya Bashani, Kwa maana msitu mnene umefyekwa!

3 Sikilizeni! Maombolezo ya wachungaji, Kwa maana fahari yao imeharibiwa.

Sikilizeni! Mingurumo ya wanasimba,*

Kwa maana mapori makubwa yaliyo kwenye kingo za Yordani yameharibiwa.

4 “Yehova Mungu wangu anasema hivi: ‘Lichunge kundi la kondoo wanaopaswa kuchinjwa,^c **5** ambao wachinjwa na wanunuzi wao^d lakini wanunuzi hao hawahesabiwi kuwa na hatia. Na wale wanaowauza^e husema, “Yehova na asifiwe, kwa maana nitakuwa tajiri.” Na wachungaji wao hawawahurumii.’^f

6 “Kwa maana sitawahurumia tena wakaaji wa nchi,’ asema Yehova. ‘Kwa hiyo nitamtia kila mtu mikononi mwa jirani yake na mfalme wake; nao wataipondaponda nchi,

11:3 *Au “wanasimba wenye manyoya marefu shingoni.”

SURA YA 10

a Isa 41:10
Isa 45:24

b Mik 4:5

SURA YA 11

c Eze 34:8

d Eze 22:25

e Ne 5:8

f Eze 34:2, 4

Safu ya 2

a Zek 11:4

b Zek 11:10, 14

c Zek 11:7

d Mt 26:14, 15
Mt 27:9
Mk 14:10, 11

e Kut 21:32

f Mt 27:5, 6
Mdo 1:18

g Zek 11:7

h 1Fa 12:19, 20
Eze 37:16

nami sitawaokoa kutoka mikononi mwao.”

7 Nami nikaanza kulichungua kundi la kondoo wanaopaswa kuchinjwa,^a kwa faida yenu, enyi kondoo mnaoteseka. Kwa hiyo nikachukua fimbo mbili, moja nikaiita Uzuri, na nyingine Muungano,^b nikaanza kulichungua kundi hilo la kondoo. **8** Nami nikawafukuza wachungaji watatu katika mwezi mmoja, kwa maana nilichoshwa nao, nao pia wakachukizwa nami. **9** Kisha nikasema: “Sitaendelea kuwachunga ninyi. Yule anayekufa na afe, na yule anayeangamia na aangamie. Na wale wanaobaki, kila mmoja wao amle mwenza-ke.” **10** Basi nikachukua fimbo yangu inayoitwa Uzuri^c na kuikatakata, na hivyo nikavunja agano langu nililokuwa nimefanya na mataifa yote. **11** Basi likavunjika siku hiyo, na kondoo walioteseka walikuwa wakinitazama walijua kwamba hilo lilikuwa neno la Yehova.

12 Kisha nikawaambia: “Ikiwa mnaona ni vema, nipeni mshahara wangu; kama sivyo, msinipe.” Basi wakanilipa* mshahara wangu, vipande 30 vya fedha.^d

13 Ndipo Yehova akaniaambia: “Vitupe katika hazina—thamani kubwa waliyonikadiria.”^e Kwa hiyo nikavichukua vipande hivyo 30 vya fedha na kuvitupa katika hazina ya nyumba ya Yehova.^f

14 Kisha nikaikatakata fimbo yangu ya pili, inayoitwa Muungano,^g na hivyo nikauvunja undugu kati ya Yuda na Israeli.^h

11:12 *Tnn., “wakanipimia.”

15 Na Yehova akaniambia: "Sasa vichukue vifaa vya mchungaji asiyejaa.^a **16** Kwa maana ninamruhusu mchungaji ainuke nchini. Hatawatunza kondoo wanaoangamia;^b hatawatafuta walio wachanga au kuwaponya waliojeruhiwa^c au kuwalisha wanaoweza kusimama. Badala yake, atamla kondoo aliyenona^d na kuwanga'oa kwato kondoo.^e

17 Ole wake mchungaji wangu asiyejaa,^f anayeliacha kundi!^g

Upanga utakata mkono wake na jicho lake la kulia.

Mkono wake utapooza kabisa,

Na jicho lake la kulia litapofuka* kabisa."

12 Tangazo:

"Neno la Yehova kuhusu Israeli," asema Yehova,

Yule aliyezitandaza mbingu,^h

Aliyeweka msingi wa dunia,ⁱ

Na kuumba roho* iliyo ndani ya mwanadamu.

2 "Tazama, ninafanya jiji la Yerusalemu liwe kikombe kinachosababisha* mataifa yote jirani yapepesuke; na jiji la Yuda litazingirwa, na pia Yerusalemu.^j **3** Siku hiyo nitafanya Yerusalemu liwe jiwe zito* kwa mataifa yote. Kwa hakika wote watakaolinyanyua watajeruhiwa vibaya;^k na mataifa yote duniani yatakusanyika kupigana na jiji hilo.^l **4** Siku hiyo," asema Yehova, "nitamtia hofu kila

11:17 *Tnn., "litafifia." 12:1 *Au "pumzi." 12:2 *Au "bakuli linalosababisha." 12:3 *Au "lenye kulemea."

SURA YA 11

a Eze 34:2, 4

b Yer 23:2
Eze 34:6
Mt 9:36

c Eze 34:21

d Mwa 31:38

e Eze 34:3, 10

f Yer 23:1
Mt 23:13

g Yoh 10:12

SURA YA 12

h Ayu 26:7
Isa 42:5

i Zb 102:25
Isa 45:18

j Zek 14:14

k Sef 3:19

l Zek 14:2, 3

Safu ya 2

a Isa 41:10
Yoe 3:16
Zek 12:8

b Isa 41:15

c Mik 4:13
Zek 9:15

d Zek 2:4

e Yer 23:6
Yoe 3:16
Zek 2:5
Zek 9:15

f Kut 14:19
Kut 23:20

g Isa 54:17
Hag 2:22

h Yoh 19:34, 37
Yoh 20:27
Ufu 1:7

farasi na kumtia wazimu yule anayempanda. Nitaika-
zia macho nyumba ya Yuda,
lakini nitampofusha kila farasi
wa mataifa. **5** Na mashehe*
wa Yuda watasema moyoni
mwao, 'Wakaaji wa Yerusalemu
ni nguvu kwetu kwa sababu
ya Yehova wa majeshi Mungu
wao.'^a **6** Siku hiyo nitawafanya
mashehe wa Yuda wawe kama
chungu cha moto kati ya kuni
na kama mwenge unaowaka
kati ya safu ya miganda iliyokatwa
ya nafaka,^b nao watayateketeza
mataifa yote jirani yaliyo upande
wa kulia na wa kushoto;^c na jiji
la Yerusalemu litakuwa tena na
wakaaji mahali pake,* huko
Yerusalemu.^d

7 "Na Yehova atayaokoa kwanza
mahema ya Yuda, ili umaridadi wa*
nyumba ya Daudi na umaridadi wa*
wakaaji wa Yerusalemu usizidi sana
ule wa Yuda. **8** Siku hiyo Yehova
atakuwa ulinzi kuwazunguka
wakaaji wa Yerusalemu;^e siku
hiyo yule anayejikwaa* kati yao
atakuwa kama Daudi, na nyumba
ya Daudi itakuwa kama Mungu,
kama malaika wa Yehova anayeta-
ngulia mbele yao.^f **9** Na siku
hiyo, kwa hakika nitayaangamiza
mataifa yote yatakatyoka
kushambulia Yerusalemu.^g

10 "Nitamimina roho ya kibalali
na dua juu ya nyumba ya Daudi
na juu ya wakaaji wa Yerusalemu,
nao watamtazama yule waliyemchoma,^h
watamwombolezea kwa sauti
kama ambavyo wangemwombolezea
mwana wa pekee;

12:5 *Shehe alikuwa mkuu wa kabila.

12:6 *Au "mahali pake panapostahili."

12:7 *Au "fahari ya." 12:8 *Au "aliye dhaifu zaidi."

watamhuzunikia sana kama ambavyo wangemhuzunikia mwana mzaliwa wa kwanza.

11 Siku hiyo kutakuwa na maombolezo makubwa Yerusalemu, kama maombolezo ya Hadadrimoni katika Nchi Tambarare ya Megido.^a **12** Na nchi itaomboleza kwa sauti, kila ukoo peke yake; ukoo wa nyumba ya Daudi peke yake, na wanawake wao peke yao; ukoo wa nyumba ya Nathani^b peke yake, na wanawake wao peke yao; **13** ukoo wa nyumba ya Lawi^c peke yake, na wanawake wao peke yao; ukoo wa Washimei^d peke yake, na wanawake wao peke yao; **14** na koo zote zinazobaki, kila ukoo peke yake, na wanawake wao peke yao.

13 “Siku hiyo kisima kitafunguliwa kwa ajili ya nyumba ya Daudi na wakaaaji wa Yerusalemu ili kuwasafisha dhambi na uchafu.^e

2 “Siku hiyo,” asema Yehova wa majeshi, “nitafuta majina ya sanamu kutoka nchini,^f nayo hayatakumbukwa tena; nami nitawaondoa kabisa manabii^g na pia roho ya uchafu kutoka nchini. **3** Na mtu akitoa unabii tena, baba yake na mama yake waliomzaa watamwambia, ‘Hutaishi, kwa sababu umesema uwongo katika jina la Yehova.’ Na baba yake na mama yake waliomzaa watamchoma kisu kwa sababu ya unabii wake.^h

4 “Siku hiyo kila nabii atonea aibu maono yake anapotabiri; nao hawatavaa vazi rasmi la manyoyaⁱ ili kudanganya. **5** Naye atasema, ‘Mimi si nabii. Mimi ni mkulima, kwa sababu mtu fulani alininunua nilipokuwa kijana.’ **6** Na mtu

SURA YA 12

a 2Fa 23:29
2Nya 35:22

b 2Sa 5:13,14
Lu 3:23,31

c Kut 6:16

d Kut 6:17
1Nya 23:10

SURA YA 13

e Eze 36:25,29

f Kut 23:13

g Kum 13:5

h Kum 13:6-9
Kum 18:20

i 2Fa 1:8
Mt 3:4

Safu ya 2

a Eze 34:23
Mik 5:4
Yoh 10:11
Ebr 13:20

b Isa 53:8
Da 9:26
Mdo 3:18

c Mt 26:31
Mt 26:55,56
Mk 14:27,50
Yoh 16:32

d Mal 3:2,3

e Yer 30:22

akimuuliza, ‘Majeraha haya uliyo nayo katikati ya mabega yako* yametoka wapi?’ atajibu, ‘Nilijeruhiwa katika nyumba ya rafiki zangu.’”[#]

7 “Ee upanga, amka umshambulie mchungaji wangu,^a

Mshambulie rafiki yangu,” asema Yehova wa majeshi.

“Mpige mchungaji,^b acha kondoo watawanyike;”^c

Nami nitageuza mkono wangu dhidi ya watu wa hali ya chini.”

8 “Na katika nchi yote,” asema Yehova,

“Theluthi mbili za watu zitaangamizwa na kuto-weka;”^{*}

Na theluthi moja itaachwa humo.

9 Na theluthi hiyo moja nitaitipisha motoni;

Nami nitawasafisha kama fedha inavyosafishwa,

Na kuwajaribu kama dhahabu inavyojaribiwa.^d

Wataliitia jina langu,

Nami nitawajibu.

Nitasema, ‘Wao ni watu wangu,’^e

Nao watasema, ‘Yehova ni Mungu wetu.’”

14 “Tazama! Siku inakuja, siku ya Yehova, wakati ambapo nyara yenu* itagawanywa miongoni mwenu. **2** Nitayakusanya mataifa yote ili yapigane vita na Yerusalemu; na jiji hilo litatekwa na nyumba zitaporwa na wanawake

13:6 *Tnn., “katikati ya mikono yako.” Yaani, kifuani au mgongoni. [#] Au “wale wanaonipenda.” **13:7** *Au “kundi la kondoo litawanyike.” **13:8** *Au “zitaku-fa.” **14:1** *Yaani, jiji linalotajwa katika mstari wa 2.

watabakwa. Na nusu ya wakaa-ji wa jiji hilo watapelekwa uhamishoni, lakini watakaobaki jijini hawataangamizwa.

3 “Yehova atatoka na kupigana vita na mataifa hayo^a kama anavyopigana katika siku ya vita.^b **4** Siku hiyo miguu yake itasimama kwenye Mlima wa Mizeituni,^c unaotazamana na jiji la Yerusalemu upande wa mashariki; na Mlima wa Mizeituni utagawanyika katikati, kuanzia mashariki* mpaka magharibi,[#] na bonde kubwa sana litatokea; na nusu ya mlima huo itaelekea kaskazini, na nusu nyingine kusini. **5** Mtakimbilia kwenye bonde la milima yangu, kwa maana bonde la milima hiyo litafika mpaka Aseli. Mtalazimika kukimbia kama mlavyokimbia kwa sababu ya tetemeko la ardhi katika siku za utawala wa Mfalme Uzia wa Yuda.^d Na Yehova Mungu wangu atakuja, na watakatifu wote watakuwa pamoja naye.^e

6 “Siku hiyo hakutakuwa na nuru yenye thamani^f—vitu vitagandishwa.* **7** Nayo itakuwa siku inayojulikana kuwa siku ya Yehova.^g Haitakuwa mchana, wala haitakuwa usiku; na jioni kutakuwa na nuru. **8** Siku hiyo maji yaliyo hai^h yatatiririka kutoka Yerusalemu,ⁱ nusu yataelekea kwenye bahari ya mashariki*^j na nusu yataelekea kwenye bahari ya magharibi.*^k Hilo litatukia wakati wa kiangazi na wa baridi kali. **9** Na Yehova atakuwa Mfalme juu ya dunia

14:4 *Au “mawio ya jua.” #Tnn., “kwenye ile bahari.” 14:6 *Au “vitakakamazwa,” kana kwamba vimekakamazwa na baridi. 14:8 *Yaani, Bahari ya Chumvi. #Yaani, Bahari ya Mediterania.

SURA YA 14

a Eze 38:23
Yoe 3:2, 14
Ufu 16:14

b Kut 15:3
2Nya 20:15

c Lu 19:29
Mdo 1:12

d Amo 1:1

e Kum 33:2
Yoe 3:11
Yud 14

f Isa 13:9, 10
Amo 5:18

g Yoe 2:31
1Th 5:2
2Pe 3:10

h Ufu 21:6
Ufu 22:17

i Yer 17:13
Eze 47:1
Yoe 3:18
Ufu 22:1

j Kum 3:17

k Yos 1:4

Safu ya 2

a Zb 97:1
Ufu 19:6

b Kum 6:4

c Isa 42:8
Isa 44:6

d Kum 1:7

e 1Fa 15:22

f 1Nya 4:24, 32

g Yer 30:18

h Yer 37:13

i Ne 3:1
Yer 31:38

j Isa 60:18
Yer 31:40

k Yer 23:6
Yer 33:16

l 2Fa 19:34, 35
Yoe 3:2

m Amu 7:22
Eze 38:21

n 2Nya 14:13
2Nya 20:25
Zek 2:8, 9

yote.^a Siku hiyo Yehova atakuwa Mungu pekee,^b na jina lake litakuwa ndilo jina pekee.^c

10 “Nchi yote itakuwa kama Araba,^d kuanzia Geba^e mpaka Rimoni^f upande wa kusini wa Yerusalemu; na jiji la Yerusalemu litainuka na kukaliwa na watu,^g kuanzia Lango la Benjamini^h mpaka kwenye Lango la Kwanza, mpaka kwenye Lango la Pembeni, na kuanzia Mnara wa Hananeliⁱ mpaka kwenye mashinikizo ya divai* ya mfalme. **11** Na watu watakaa jijini humo; hakutakuwa tena na laana ya uhari-bifu,^j na watu watakaa Yerusalemu kwa usalama.^k

12 “Na huu ndio ugonjwa hatari ambao Yehova atawaletea watu wote wanaopigana vita na Yerusalemu!^l Miili yao itaoza wakiwa wamesimama, macho yao yataoza ya kiwa kwenye matundu yake, na ndimi zao zitaoza vinywani mwao.

13 “Siku hiyo msukosuko kutoka kwa Yehova utae-nea sana miongoni mwao; na kila mtu ataukamata mkono wa mwenzake, na mko-no wake utashambulia mko-no wa mwenzake.*^m **14** Watu wa Yuda pia watashiriki katika vita huko Yerusalemu; na utajiri wa mataifa yote jirani utakusanywa, dhahabu na fedha na mavazi kwa wingi sana.ⁿ

15 “Na ugonjwa hatari wa aina hiyo utawashambulia pia farasi, nyumbu, ngamia, punda, na mifugo yote iliyo kati-ka kambi hizo.

16 “Kila mtu atakayebaki

14:10 *Au “mitungi ya kushinikizia divai.” 14:13 *Au “mtu atamshambulia mwenzake.”

kutoka katika mataifa yote yatakayoshambulia Yerusalemu atapanda mwaka baada ya mwaka^a kwenda Yerusalemu kumwinamia* Mfalme, Yehova wa majeshi,^b na kusherehekea Sherehe ya Vibanda.^{#c} **17** Lakini ikiwa taifa lolote miongoni mwa mataifa yaliyo duniani halitapanda kwenenda Yerusalemu kumwinamia Mfalme, Yehova wa majeshi, mvua haitanyesha katika taifa hilo.^d **18** Na ikiwa taifa la Misri halitapanda kwenda Yerusalemu na kuingia humo, halitapata mvua. Badala yake, litashambuliwa na ugonjwa hatari ambao Yehova anauleta kwa mataifa ambayo hayapandi kwenda kusherehekea Sherehe ya Vibanda. **19** Hiyo ndiyo itakayokuwa adhabu kwa sababu ya dha-

14:16 *Au "kumwabudu." #Au "Vibanda ywa Muda."

SURA YA 14

a Isa 66:23

b Zb 86:9

c Law 23:34
Ne 8:14, 15

d Isa 60:12

Safu ya 2

a Kut 28:36
Kut 39:30

b 1Sa 2:13, 14

c Kut 25:29
Hes 4:7

d Eze 44:9

mbi ya Misri na dhambi ya mataifa yote ambayo hayataapanda kwenda kusherehekea Sherehe ya Vibanda.

20 "Siku hiyo maneno 'Uta-katifu ni wa Yehova!'^a yataandikwa kwenye kengele za farasi. Na vyungu vya kupikia^{*b} vilivyo katika nyumba ya Yehova vitakuwa kama mabakuli^c yaliyo mbele ya madhabahu. **21** Na kila chungu cha kupikia* kilicho Yerusalemu na Yuda kitakuwa kitakatifu na kitakuwa cha Yehova wa majeshi, na wale wote wanaotoa dhabihu wataingia na kutumia baadhi ya vyungu hivyo kuchemshia. Siku hiyo hakitakuwa tena na Mkanaani[#] katika nyumba ya Yehova wa majeshi."^d

14:20 *Au "vyungu vya kupikia vye-nye mdomo mpana." **14:21** *Au "chungu cha kupikia chenye mdomo mpana." #Au labda, "mfanyabiashara."

MALAKI

YALIYOMO

- 1 Yehova anawapenda watu wake (1-5)
Makuhani watoa dhabihu zisizofaa (6-14)
Jina la Mungu litakuwa kuu miongoni mwa mataifa (11)
- 2 Makuhani washindwa kuwafundisha watu (1-9)
Midomo ya kuhani inapaswa kulinda ujuzi (7)
Watu wawataliki wake zao bila msingi (10-17)
"Ninachukia talaka,' asema Yehova" (16)
- 3 Bwana wa kweli aja kutakasa hekalu lake (1-5)
Mjumbe wa agano (1)

- Washauriwa wamrudie Yehova (6-12)
Yehova habadiliki (6)
"Nirudieni, nami nitawarudia" (7)
'Leteni sehemu yote ya kumi, na Yehova atawamwagia baraka' (10)
Mwadilifu na mwovu (13-18)
Majina yaandikwa katika kitabu cha kumbukumbu cha Mungu (16)
Tofauti kati ya mwadilifu na mwovu (18)
- 4 Kuja kwa Eliya kabla ya siku ya Yehova (1-6)
"Jua la uadilifu litawaangazia" (2)

1 Tangazo:
Neno la Yehova kwa Waisraeli kupitia Malaki:*

2 “Nimewaonyesha ninyi watu upendo,”^a asema Yehova.

Lakini mnauliza: “Umetuonyesha je upendo?”

“Je, Esau hakuwa ndugu ya Yakobo?”^b asema Yehova.

“Lakini nilimpenda Yakobo, **3** nami nikamchukia Esau;^c nikafanya milima yake kuwa ukiwa^d na urithi wake nika-waachia mbwamwitu wa nyikani.”^e

4 “Ingawa Waedomu wanasema, ‘Tumevunjwavunjwa, lakini tutarudi na kujenga tena magofu,’ Yehova wa majeshi anasema hivi: ‘Watajenga, lakini nitabomoa, nao wataitwa “eneo la uovu” na “watu ambao Yehova amewahukumu milele.”^f **5** Macho yenu wenyewe yataona hilo, nanyi mtasema: “Yehova na atukuzwe katika eneo la Israeli.””

6 “Mwana humheshimu baba yake,^g na mtumishi bwana wake. Basi ikiwa mimi ni baba,^h iko wapi heshima ninayostahili?ⁱ Na ikiwa mimi ni bwana,^{*} iko wapi hofu^z ninayostahili? Mimi Yehova wa majeshi ninawauliza ninyi makuhani mnaolidharau jina langu.^j

“Lakini mnauliza: “Tumelidharau jina lako kwa njia gani?””

7 “Kwa kutoa chakula kilichochofuliwa* juu ya madhabu yangu.’

“Nanyi mnauliza: “Tumekuchafua jinsi gani?””

1:1 *Maana yake “Mjumbe Wangu.” 1:6 *Au “bwana mkubwa.” ^zAu “heshima.” 1:7 *Tnn., “mkate uliotiwa unajisi.”

SURA YA 1

a Kum 10:15

b Mwa 25:25, 26

c Ro 9:13

d Yer 49:20
Yoe 3:19

e Isa 34:10, 13

f Isa 34:5
Oba 18

g Kut 20:12

h Kut 4:22

i Isa 1:2

j Eze 22:26

Safu ya 2

a Eze 41:21, 22
Iko 10:21b Law 22:20, 22
Kum 15:21

c 2Nya 23:4

d Yer 6:13
Mik 3:11e Isa 1:11
Yer 6:20f Zb 113:3
Isa 45:6
Isa 59:19g Zb 22:27
Sef 3:9
Mt 28:19
Ufu 15:4

h Eze 22:26

i Mal 1:7

“Kwa kusema: “Meza ya Yehova^a ni kitu cha kudharauliwa.” **8** Na mnapomtoa mnyama kipofu kuwa dhahihu, mnasema: “Si vibaya.” Na mnapomtoa mnyama kilema au mgonjwa mnasema: “Si vibaya.””^b

“Tafadhali, jaribuni kumtolea gavana wenu vitu hivyo. Je, atapendezwa nanyi au kuwapokea ninyi kwa kibali?” asema Yehova wa majeshi.

9 “Na sasa, tafadhali, msihini* Mungu ili atuonyeshe kibali. Mkitoa dhahihu za aina hiyo kwa mikono yenu, je, atampokea yeyote kati yenu kwa kibali?” auliza Yehova wa majeshi.

10 “Na ni nani miongoni mwenu aliye tayari kufunga milango?”^c Kwa maana hata hamtawasha moto kwenye madhabahu yangu bila malipo.^d Sipendezwi nanyi,” asema Yehova wa majeshi, “nami sipendezwi na zawadi yoyote kutoka mikononi mwenu.”^e

11 “Kwa maana tangu juu ya lipapochomoza mpaka linapotua,* jina langu litakuwa kuu miongoni mwa mataifa.^f Kila mahali dhahihu zitafukizwa moshi, na matoleo yatatolewa kwa jina langu, yakiwa zawadi safi; kwa sababu jina langu litakuwa kuu miongoni mwa mataifa,”^g asema Yehova wa majeshi.

12 “Lakini ninyi mnalitia unajisi*^h kwa kusema, ‘Meza ya Yehova imechafuliwa, matunda yake, chakula chake, ni kitu cha kudharauliwa.’ⁱ

1:9 *Tnn., “utulizeni uso wa.” 1:10 *Inaonekana ni wajibu wa kufunga milango ya hekalu. 1:11 *Au “kutoka mashariki mpaka magharibi.” 1:12 *Au labda, “mnanitia unajisi.”

13 Pia mnasema, "Tazama! Inachosha kwelikweli!" na kwa pua zenu mnaishushia pumzi kwa dharau," asema Yehova wa majeshi. "Nanyi mnaleta wanyama walioibwa, vilema, na wagonjwa. Naam, mnaleta vitu hivyo kuwa zawadi! Je, niikubali kutoka mikononi mwenu?"^a auliza Yehova.

14 "Amelaaniwa mtu mjanja aliye na mnyama asiye na kasoro katika kundi lake, lakini anaapa na kumtolea Yehova dhabihu ya mnyama mwenye kasoro.* Kwa maana mimi ni Mfalme mkuu,"^b asema Yehova wa majeshi, "na jina langu litakuwa lenye kuogopesha miongoni mwa mataifa."^c

2 "Na sasa, enyi makuhani, amri hii inawahusu.^d **2** Mkikataa kusikiliza na kuitia moyoni mwenu ili kulitukuza jina langu," asema Yehova wa majeshi, "nitawaletea laana,^e nami nitabadili baraka zenu ziwe laana.^f Naam, nimebadili baraka ziwe laana, kwa sababu hamwitii moyoni mwenu."

3 "Tazameni! Nitaharibu* mbegu zenu zilizopandwa kwa sababu yenu,^g nami nitawapaka kinyesi cha wanyama usoni, kinyesi cha sherehe zenu; nanyi mtabebwa na kupeleleka kwenye kinyesi hicho.* **4** Ndipo mtakapojua kwamba nimewapa amri hii ili agano langu pamoja na Lawi liendeleo,"^h asema Yehova wa majeshi.

5 "Agano langu pamoja naye lilikuwa la uzima na amani, ambalo nilimpa, pamoja na

1:14 *Au "dosari." 2:3 *Tnn., "Nitake-mea." *Yaani, mahali ambapo kinyesi cha wanyama wa dhabihu kilitupwa.

SURA YA 1

a Law 22:20, 22
Kum 15:21
Kum 17:1

b Zb 47:2
Yer 10:10

c Ufu 15:4

SURA YA 2

d Mal 1:6

e Law 26:14-17
Kum 28:15

f Hag 1:11

g Yoe 1:17

h Kut 40:12, 15
Hes 3:6
Hes 18:23
Eze 44:15, 16

Safu ya 2

a 2Nya 17:8, 9

b Kut 32:26

c Kum 24:8
2Nya 15:3
Ne 8:7, 8
Eze 44:23, 24

d Lu 11:52

e Ne 13:29

f Law 19:15
Kum 1:17
Kum 16:19

g Mal 1:6
1Ko 8:6

h Ne 5:8

i Law 20:26

j Kum 7:1, 3
Amu 3:5, 6
1Fa 11:1, 2
Ne 13:23

hofu.* Aliniogopa, naam, aliliheshimu jina langu. **6** Sheria ya kweli ilikuwa* kinywani mwake,^a na ukosefu wa uadilifu haukupatikana midomoni mwake. Alitembea pamoja nami kwa amani na kwa unyoofu,^b naye aliwageuza wengi kutoka katika uovu. **7** Kwa maana midomo ya kuhani inapaswa kulinda ujuzi, na watu wanapaswa kutafuta sheria* kutoka kinywani mwake,^c kwa sababu yeye ni mjumbe wa Yehova wa majeshi.

8 "Lakini ninyi wenyewe mmegeuka na kuiacha njia. Mmewafanya wengi wajikwae kuhusiana na sheria.*^d Mmeliharibu agano la Lawi,"^e asema Yehova wa majeshi. **9** "Kwa hiyo nitawafanya ninyi mdhauruliwe na kuwa duni mbele ya watu wote, kwa sababu hamkushika njia zangu badala yake mliitekeleza sheria kwa upendeleo."*^f

10 "Je, sisi sote hatuna baba mmoja?^g Je, hatukuumbwa na Mungu yuleule? Basi kwa nini tunatendeani kwa hila,^h na kulitia unajisi agano la mababu zetu? **11** Yuda ametenda kwa hila, na jambo fulani lenye kuchukiza limetendwa Israeli na Yerusalemu; kwa maana Yuda ameutia unajisi utakatifu wa* Yehova,ⁱ Anaoupenda, naye amemchukua binti ya mungu wa kigeni kuwa bibi haruru.^j **12** Yehova atamwanga-miza kutoka katika mahema ya Yakobo mtu yeyote anaye-

2:5 *Au "heshima, adhama." 2:6 *Au "Mafundisho ya kweli yalikuwa." 2:7 *Au "mafundisho." 2:8 *Au labda, "kwa mafundisho yenu." 2:9 *Au "ubaguzi." 2:11 *Au labda, "ametia unajisi mahali patakifu pa."

fanya hivyo, mtu yeyote yule,* hata ingawa anamtolea zawadi Yehova wa majeshi.”^a

13 “Na kuna jambo lingine* mnalotenda linalofanya madhabahu ya Yehova ifuni-kwe kwa machozi na kilio na maombolezo, hivi kwamba hakazii tena uangalifu zawadi mnyamtolea wala kutazama kwa kibali kitu chocho- te kinachotoka mikononi mwenu.^b **14** Nanyi mnauliza, ‘Kwa sababu gani?’ Ni kwa sababu Yehova amekuwa shahidi kati yako na mke wa ujana wako, ambaye umemtendea kwa hila, ingawa yeye ni mwenzi wako na mke wako kupitia agano.*^c **15** Lakini kuna mtu ambaye hakufanya hivyo, kwa sababu ya roho iliyobaki ndani yake. Na mtu huyo alikuwa akitafuta nini? Uzao wa* Mungu. Basi jilindeni kuhusiana na roho yenu, na usimtendee kwa hila mke wa ujana wako. **16** Kwa maana ninachukia* talaka,”^d asema Yehova Mungu wa Israeli, “na pia yule anayefunika vazi lake kwa ukatili,”^e asema Yehova wa majeshi. “Nanyi jilindeni wenyewe kuhusiana na roho yenu, na hampaswi kutenda kwa hila.”^e

17 “Mmemchosha Yehova kwa maneno yenu.^f Lakini mnauliza, ‘Tumemchoshaje?’ Kwa kusema, ‘Kila mtu anayetenda maovu ni mwema machoni pa Yehova, naye hupe- ndezwa na mtu huyo,’^g au kwa kuuliza, ‘Yuko wapi Mungu wa haki?’”

2:12 *Tnn., “yule aliye macho na yule anayejibu.” 2:13 *Tnn., “la pili.” 2:14 *Au “mke wako halali.” 2:15 *Tnn., “Mbegu ya.” 2:16 *Tnn., “anachukia.”^e Tnn., “anayetenda ukatili.”

SURA YA 2

a 1Sa 15:22

b Met 21:27

c Met 5:18-20
Mt 19:4-6d Mwa 2:24
Mt 5:32
Mt 19:8, 9
Mk 10:5-9

e Mal 2:10

f Isa 1:14, 15

g Eze 18:29

Safu ya 2

SURA YA 3

a Mt 3:1-3
Mt 11:7, 10
Mk 1:2-4
Lu 1:76
Yoh 1:6, 23
Yoh 3:28

b Zb 11:4

c Isa 1:25
Yer 2:22d Zb 66:10
Met 25:4
Zek 13:9

e 2Nya 7:1

f Kum 18:10, 12

g Kut 20:7

h Met 14:31
Yak 5:4i Kum 24:17
Isa 1:17
Yak 1:27j Kut 23:9
Zek 7:10k Isa 43:10
Isa 46:4
Yak 1:17

3 “Tazama! Ninamtuma mju- mbe wangu, naye atafu- ngua* njia mbele yangu.^a Na ghafla Bwana wa kweli, mna- yemtafuta, atakuja katika he- kalu lake;^b na mjumbe wa agano atakuja, mnyayende- zwa naye. Tazama! Kwa haki- ka atakuja,” asema Yehova wa majeshi.

2 “Lakini ni nani atakaye- stahimili siku atakayokuja, na ni nani atakayeweza ku- simama atakapotokea? Kwa maana atakuwa kama moto wa msafishaji wa madini na kama sabuni^c ya wafuaji wa nguo. **3** Naye ataketi kama msafishaji na mtakasaji wa fe- dha,^d naye atawatakasa wana wa Lawi; atawasafisha kama dhahabu na kama fedha, nao hakika watakuwa watu wanao- mtolea Yehova zawadi kwa u- dilifu. **4** Na kwa kweli zawadi ya Yuda na Yerusalemu ita- mpendeza* Yehova, kama ili- vyokuwa katika siku za kale na kama ilivyokuwa katika miaka ya zamani za kale.^e

5 “Nitawakaribia ili niwa- hukumu, nami nitakuwa sha- hidi asiyesita* dhidi ya wa- lozi,^f dhidi ya wazinzi, dhidi ya watu wanaotoa viapo vya uwongo,^g dhidi ya wale wa- naomlaghai kibarua,^h mjane, na yatima,ⁱ na dhidi ya wale wanaokataa kumsaidia^Δ mge- ni.^j Watu hao hawaniogopi,” asema Yehova wa majeshi.

6 “Kwa maana mimi ni Ye- hova; sibandiliki.*^k Nanyi ni wana wa Yakobo; bado ha- mjaangamia. **7** Tangu siku

3:1 *Au “atatayarisha.” 3:4 *Au “itamridhisha.” 3:5 *Tnn., “mwepesi.”^e Tnn., “mtoto asiye na baba.”^Δ Au “wanaomnyima haki.” 3:6 *Au “sijabadi- lika.”

za mababu zenu mmegeuka na kuacha masharti yangu nanyi hamjayashika.^a Nirudieni, nami nitawarudia,”^b asema Yehova wa majeshi.

Lakini mnauliza: “Tukurudie jinsi gani?”

8 “Je, mwanadamu anaweza kumwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia.”

Nanyi mnauliza: “Tumekuibia jinsi gani?”

“Katika sehemu za kumi na michango. **9** Kwa hakika mmelaaniwa,* kwa maana mnaniibia—naam, taifa zima linafanya hivyo. **10** Leteni ghalani sehemu yote ya* kumi,^c ili kuwe na chakula nyumbani mwangu;^d tafadhali, nijaribuni kwa njia hii,” asema Yehova wa majeshi, “mwone kama sitawafungulia malango ya mbinguni ya mafuriko^e na kuwamwagia baraka hivi kwamba hamtakosa chochote.”^f

11 “Na kwa ajili yenu nitamkemea yule anayenyafua,* naye hataharibu mazao ya nchi yenu, wala mzabibu wa shamba lenu hautakosa matunda,”^g asema Yehova wa majeshi.

12 “Mataifa yote yatalazimika kuwatangaza ninyi kuwa wenye furaha,^h kwa maana mtakuwa nchi ya kupendeza,” asema Yehova wa majeshi.

13 “Maneno yenu dhidi yangu yamekuwa makali,” asema Yehova.

Nanyi mnauliza: “Ni katika njia gani tumesema maneno makali dhidi yako miongoni mwetu?”ⁱ

3:9 *Au labda, “Kwa laana mnanilaani.”
3:10 *Au “sehemu zote za.” 3:11 *Inaonekana ni pigo la wadudu.

SURA YA 3

a Kum 9:7
Mdo 7:51

b Yer 3:12
Zek 1:3
Yak 4:8

c Law 27:30
Kum 14:28

d 2Nya 31:11
Ne 12:44
Ne 13:10

e Kum 28:12

f Law 26:10
2Nya 31:10
Met 3:9, 10

g Kum 11:14
Zek 8:12

h Isa 61:9

i Mal 1:6

Safu ya 2

a Ayu 21:14, 15
Zb 73:13, 14
Isa 58:3
Sef 1:12

b Yer 12:1

c Zb 56:8
Zb 69:28

d Isa 26:8

e Yer 31:33

f Isa 62:3
1Pe 2:9

g Zb 103:13

h Zb 58:10, 11

SURA YA 4

i Sef 2:2
2Pe 3:7

14 “Mnasema, ‘Hakuna faida yoyote ya kumtumikia Mungu.’^a Tumefaidikaje kwa kutimiza wajibu wetu kwake na kutembea kwa huzuni mbele za Yehova wa majeshi?”

15 Sasa tunawaona watu wenye kimbelebele kuwa wenye furaha. Pia, watu wanaotenda maovu wanafanikiwa.^b Wanathubutu kumjaribu Mungu, nao hawaadhibiwi.”

16 Wakati huo wale wanaomwogopa Yehova walizungumza kila mmoja na mwenzake, na Yehova akaendelea kuwakazia uangalifu na kusikiliza. Na kitabu cha kumbukumbu kikaandikwa mbele zake^c kwa ajili ya wale wanaomwogopa Yehova na wale wanaolitafakari* jina lake.^d

17 “Nao watakuwa wangu,”^e asema Yehova wa majeshi, “siku nitakayotokeza mali ya pekee.*^f Nitawahurumia, kama mwanamume anavyomhurumia mwana wake anayemtumikia.^g **18** Nanyi mtaona tena tofauti kati ya mtu mwadilifu na mtu mwovu,^h kati ya yule anayemtumikia Mungu na yule asiyemtumikia.”

4 “Kwa maana tazama! siku inakuja inayowaka kama tanuru,ⁱ wakati ambapo wote wenye kimbelebele na wote wanaotenda uovu watakuwa kama majani makavu. Siku hiyo inayokuja kwa hakika itawateketeza,” asema Yehova wa majeshi, “nayo haitawachia mzizi wala tawi. **2** Lakini ninyi mnaoliheshimu* jina

3:16 *Au “wanaolifikiria.” Au labda, “wanaolithamini.” 3:17 *Au “mali ninayothamini sana.” 4:2 *Tnn., “mnaoliogopa.”

langu, jua la uadilifu litawaangazia likiwa na miale inayoponya;* nanyi mtaruka huku na huku kama ndama waliononeshwa.”

3 “Nanyi mtawakanyagakanyaga waovu chini ya miguu yenu, kwa sababu watakuwa kama mavumbi chini ya nyayo zenu siku nitakayochukua hatua,” asema Yehova wa majeshi.

4:2 * Tnn., “mabawa yanayoponya.”

Safu ya 2

SURA YA 4

a Kum 4:5

b Mt 11:13, 14
Mk 9:11, 12

c Yoe 2:31
Mdo 2:20
2Pe 3:10

d Lu 1:17

4 “Kumbukeni Sheria ya Musa mtumishi wangu, masharti na maamuzi niliyoamuru kule Horebu ili Waisraeli wote wayatii.^a

5 “Tazama! Namtuma kwenu nabii Eliya^b kabla haijaja ile siku kuu ya Yehova yenye kuogopesha.^c **6** Naye ataigeuza mioyo ya akina baba iwarudie wana,^d na mioyo ya wana iwarudie akina baba, ili nisije na kuipiga dunia, na hivyo kuinganamiza.”

(Mwisho wa tafsiri ya Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu.
Ifuatayo ni tafsiri ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo)

KULINGANA NA
MATHAYO

YALIYOMO

- 1 Ukoo wa Yesu Kristo (1-17)
Yesu azaliwa (18-25)
- 2 Wanajimu wamtembelea Yesu (1-12)
Kukimbilia Misri (13-15)
Herode awaua wavulana wadogo (16-18)
Kurudi Nazareti (19-23)
- 3 Yohana Mbatizaji ahubiri (1-12)
Yesu abatizwa (13-17)
- 4 Ibilisi amjaribu Yesu (1-11)
Yesu aanza kuhubiri Galilaya (12-17)
Wanafunzi wa kwanza
wachaguliwa (18-22)
Yesu ahubiri, afundisha, na
kuponya (23-25)
- 5 MAHUBIRI YA MLIMANI (1-48)
Yesu aanza kufundisha mlimani (1, 2)
Mambo tisa yanayoleta furaha (3-12)
Chumvi na nuru (13-16)
Yesu alikuja kutimiza Sheria (17-20)
Mashauri kuhusu hasira (21-26),
uzinzi (27-30), talaka (31, 32),
viapo (33-37), kulipiza kisasi (38-42),
kupenda adui (43-48)
- 6 MAHUBIRI YA MLIMANI (1-34)
Msijionyeshe kuwa waadilifu (1-4)
Jinsi ya kusali (5-15)
Sala ya mfano (9-13)
Kufunga (16-18)
Hazina duniani na mbinguni (19-24)
Acheni kuhangaika (25-34)
Endeleeni kuatafuta kwanza
Ufalme (33)
- 7 MAHUBIRI YA MLIMANI (1-27)
Acheni kuhukumu (1-6)
Endeleeni kuomba, kutafuta,
kupiga hodi (7-11)
Kanuni Bora (12)
Lango jembamba (13, 14)
Watajulikana kwa matunda yao (15-23)
Nyumba iliyo juu ya mwamba,
nyumba iliyo juu ya mchanga (24-27)
Umati washangazwa na njia ya Yesu ya
kufundisha (28, 29)
- 8 Mtu mwenye ukoma aponywa (1-4)
Ofisa wa jeshi mwenye imani (5-13)
Yesu aponya wengi Kapernaumu (14-17)
Jinsi ya kumfuata Yesu (18-22)
Yesu atuliza dhoruba (23-27)
Yesu awaruhusu roho waovu waingie
katika nguruwe (28-34)
- 9 Yesu amponya mtu aliyepooza (1-8)
Yesu amwita Mathayo (9-13)
Swali kuhusu kufunga (14-17)
Binti ya Yairo; mwanamke agusa vazi la
nje la Yesu (18-26)
Yesu aponya vipofu na mabubu (27-34)
Mavuno ni mengi lakini wafanyakazi ni
wachache (35-38)
- 10 Mitume 12 (1-4)
Maagizo kwa ajili ya huduma (5-15)
Wanafunzi watateswa (16-25)
Mwogope Mungu, si wanadamu (26-31)
Sikuleta amani, bali upanga (32-39)
Kuwakaribisha wanafunzi wa
Yesu (40-42)
- 11 Yohana Mbatizaji asifiwa (1-15)
Kizazi kisicho na imani
chashutumiwa (16-24)
Yesu amsifu Baba yake
kwa kuwafunulia mambo
wanyenyekevu (25-27)
Nira ya Yesu inaburudisha (28-30)
- 12 Yesu ndiye "Bwana wa Sabato" (1-8)
Mtu mwenye mkono uliopooza
aponywa (9-14)
Mtumishi mpendwa wa Mungu (15-21)
Atumia roho takatifu kuwafukuza roho
waovu (22-30)
Dhambi isiyosamehewa (31, 32)
Mti hujulikana kwa matunda yake (33-37)
Ishara ya Yona (38-42)
Roho mwovu anaporudi (43-45)
Mama na ndugu za Yesu (46-50)
- 13 MIFANO KUHUSU UFALME (1-52)
Mpandaji (1-9)
Kwa nini Yesu alitumia mifano? (10-17)
Mfano wa mpandaji
wafafanuliwa (18-23)
Ngano na magugu (24-30)
Mbegu ya haradali na chachu (31-33)

- Yesu atumia mifano, atimiza unabii (34, 35)
 Mfano wa ngano na magugu wafanuliwa (36-43)
 Hazina iliyofichwa na lulu nzuri (44-46)
 Wavu wa kukokota (47-50)
 Hazina mpya na za zamani (51, 52)
 Yesu akataliwa katika eneo la nyumbani kwao (53-58)
- 14 Yohana Mbatizaji akatwa kichwa (1-12)
 Yesu alisha wanaume 5,000 (13-21)
 Yesu atembea juu ya maji (22-33)
 Yesu awaponya watu huko Genesareti (34-36)
- 15 Yesu afunua mapokeo ya wanadamu (1-9)
 Mtu huchafuliwa na kinachotoka moyoni (10-20)
 Imani kubwa ya mwanamke Mfoinike (21-28)
 Yesu aponya magonjwa mengi (29-31)
 Yesu alisha wanaume 4,000 (32-39)
- 16 Waomba ishara (1-4)
 Chachu ya Mafarisayo na Masadukayo (5-12)
 Funguo za Ufalme (13-20)
 Kutaniko lajengwa juu ya mwamba (18)
 Kifo cha Yesu chatabiriwa (21-23)
 Wanafunzi wa kweli (24-28)
- 17 Yesu ageuka sura (1-13)
 Imani kama mbegu ya haradali (14-21)
 Kifo cha Yesu chatabiriwa tena (22, 23)
 Walipa kodi kwa sarafu iliyotolewa kinywani mwa samaki (24-27)
- 18 Aliye mkuu zaidi katika Ufalme (1-6)
 Vikwazo (7-11)
 Mfano wa kondoo aliyepotea (12-14)
 Jinsi ya kumpata ndugu yako (15-20)
 Mfano wa mtumwa aliyekosa kusamehe (21-35)
- 19 Ndoa na talaka (1-9)
 Zawadi ya useja (10-12)
 Yesu awabariki watoto (13-15)
 Swali la mwanamume kijana tajiri (16-24)
 Kujidhabihu kwa ajili ya Ufalme (25-30)
- 20 Wafanyakazi katika shamba la mizabibu wapokea mshahara unaolingana (1-16)
 Kifo cha Yesu chatabiriwa tena (17-19)
- Ombi la kupewa vyeo katika Ufalme (20-28)
 Yesu atoa fidia kwa ajili ya wengi (28)
 Wanaume wawili vipofu waponywa (29-34)
- 21 Yesu aingia kwa kishindo (1-11)
 Yesu asafisha hekalu (12-17)
 Mtini walaaniwa (18-22)
 Wataka kujua chanzo cha mamlaka ya Yesu (23-27)
 Mfano wa wana wawili (28-32)
 Mfano wa wakulima wauaji (33-46)
 Jiwe kuu la pembeni lakataliwa (42)
- 22 Mfano wa karamu ya ndoa (1-14)
 Mungu na Kaisari (15-22)
 Swali kuhusu ufufuo (23-33)
 Amri mbili zilizo kuu zaidi (34-40)
 Je, Kristo ni mwana wa Daudi? (41-46)
- 23 Msiwaige waandishi na Mafarisayo (1-12)
 Ole kwa waandishi na Mafarisayo (13-36)
 Yesu aombolezea Yerusalemu (37-39)
- 24 ISHARA YA KUWAPO KWA KRISTO (1-51)
 Vita, njaa, matetemeko ya ardhi (7)
 Habari njema itahubiriwa (14)
 Dhiki kuu (21, 22)
 Ishara ya Mwana wa binadamu (30)
 Mtini (32-34)
 Kama siku za Noa (37-39)
 Endeeleni kukesha (42-44)
 Mtumwa mwaminifu na mtumwa mwovu (45-51)
- 25 ISHARA YA KUWAPO KWA KRISTO (1-46)
 Mfano wa mabikira kumi (1-13)
 Mfano wa talanta (14-30)
 Kondoo na mbuzi (31-46)
- 26 Makuhani wapanga njama ya kumuua Yesu (1-5)
 Yesu amiminiwa mafuta yenye manukato (6-13)
 Pasaka ya mwisho na kusalitiwa (14-25)
 Mlo wa Jioni wa Bwana waanzishwa (26-30)
 Yesu atabiri kwamba Petro atamkana (31-35)
 Yesu asali huko Gethsemane (36-46)
 Yesu akamatwa (47-56)
 Kesi mbele ya Sanhedrini (57-68)
 Petro amkana Yesu (69-75)
- 27 Yesu akabidhiwa kwa Pilato (1, 2)
 Yuda ajinyonga (3-10)

Yesu mbele ya Pilato (11-26)
 Adihakiwa hadharani (27-31)
 Atundikwa kwenye mti huko
 Golgotha (32-44)
 Yesu afa (45-56)
 Yesu azikwa (57-61)
 Kaburi lawekewa ulinzi mkali (62-66)

28 Yesu afufuliwa (1-10)
 Askari wapewa rushwa ili waseme
 uwongo (11-15)
 Agizo la kufanya watu kuwa
 wanafunzi (16-20)

1 Kitabu cha historia ya*
 Yesu Kristo,[#] mwana wa
 Daudi,^a mwana wa Abrahamu.^b

2 Abrahamu akawa baba ya
 Isaka;^c

Isaka akawa baba ya
 Yakobo;^d

Yakobo akawa baba ya
 Yuda^e na ndugu zake;

3 Yuda akawa baba ya
 Perezi na Zera^f kupitia
 Tamari;

Perezi akawa baba ya
 Hezroni;^g

Hezroni akawa baba ya
 Ramu;^h

4 Ramu akawa baba ya
 Aminadabu;
 Aminadabu akawa baba
 ya Nashoni;ⁱ

Nashoni akawa baba ya
 Salmoni;

5 Salmoni akawa baba ya
 Boazi kupitia Rahabu;^j
 Boazi akawa baba ya
 Obedi kupitia Ruthu;^k
 Obedi akawa baba ya
 Yese;^l

6 Yese akawa baba ya Mfal-
 me Daudi.^m

Daudi akawa baba
 ya Sulemaniⁿ kupitia
 mke wa Uria;

SURA YA 1

a 1Nya 17:11

Mt 9:27

Lu 1:32, 33

b Mwa 22:18

c Mwa 21:3

d Mwa 25:26

1Nya 1:34

e Mwa 29:35

f Mwa 38:29, 30

g Ru 4:18-22

h 1Nya 2:9

i 1Nya 2:10, 11

j Yos 2:1

k Ru 4:13

l 1Nya 2:12

m 1Nya 2:13, 15

n 2Sa 12:24

1Nya 3:5

Safu ya 2

a 1Fa 11:43

b 1Nya 3:10-19

2Nya 14:1

c 1Fa 15:24

d 2Nya 21:1

e 2Fa 15:32

f 2Fa 15:38

g 2Fa 18:1

h 2Fa 20:21

i 2Nya 33:20

j 2Fa 21:24

k 2Fa 23:34

l 1Nya 3:15, 16

m 2Fa 24:12, 15

2Nya 36:9, 10

n Ezr 3:2

Ne 12:1

7 Sulemani akawa baba ya
 Rehoboamu;^a

Rehoboamu akawa baba
 ya Abiya;

Abiya akawa baba ya Asa;^b

8 Asa akawa baba ya Yeho-
 shafati;^c

Yehoshafati akawa baba
 ya Yehoram;^d

Yehoram akawa baba
 ya Uzia;

9 Uzia akawa baba ya
 Yothamu;^e

Yothamu akawa baba ya
 Ahazi;^f

Ahazi akawa baba ya
 Hezekia;^g

10 Hezekia akawa baba ya
 Manase;^h

Manase akawa baba ya
 Amoni;ⁱ

Amoni akawa baba ya
 Yosia;^j

11 Yosia^k akawa baba ya
 Yekonia^l na ndugu zake,
 wakati wa kupelekwa
 uhamishoni Babiloni.^m

12 Baada ya kupelekwa
 uhamishoni Babiloni,
 Yekonia akawa baba ya
 Shealtieli;

Shealtieli akawa baba ya
 Zerubabeli;ⁿ

13 Zerubabeli akawa baba ya
 Abiudi;

Abiudi akawa baba ya
 Eliakimu;

1:1 *Au "ukoo wa." # Au "Masihi; Mtiwa-
 mafuta."

- Eliakimu akawa baba ya Azori;
- 14** Azori akawa baba ya Sadoki; Sadoki akawa baba ya Akimu; Akimu akawa baba ya Eliudi;
- 15** Eliudi akawa baba ya Eleazari; Eleazari akawa baba ya Mathani; Mathani akawa baba ya Yakobo;
- 16** Yakobo akawa baba ya Yosefu mume wa Maria, aliyemzaa Yesu,^a aitwaye Kristo.^b

17 Kuanzia Abrahamu mpaka Daudi kulikuwa na vizazi 14; kuanzia Daudi mpaka wakati wa kupelekwa uhamishoni Babiloni, vizazi 14; kuanzia wakati wa kupelekwa uhamishoni Babiloni mpaka Kristo, vizazi 14.

18 Basi kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulikuwa hivi: Maria mama ya Yesu alichumbiwa na Yosefu, lakini kabla hawajafunga ndoa akapata mimba kupitia roho takatifu.*^c

19 Hata hivyo, kwa sababu Yosefu mume wake alikuwa mwadilifu na hakutaka kumwaibisha hadharani, alikusudia kumtaliki kisiri.^d

20 Lakini baada ya kufikiria mambo hayo, tazama! malaika wa Yehova* alimtokea katika ndoto na kumwambia: "Yosefu, mwana wa Daudi, usiogope kumpeleka Maria mke wako

1:18 *Au "nguvu ya utendaji." **1:20** *Hii ndiyo mara ya kwanza, kati ya mara 237 katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo ambapo jina la Mungu, Yehova, linapatikana katika toleo hili. Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 1

a Mt 13:55
Mk 6:3

b Lu 3:23-38

c Lu 1:35

d Kum 24:1

Safu ya 2

a Lu 1:35

b Mt 1:25
Lu 1:31

c Lu 2:30
Yoh 1:29
Mdo 4:12
Mdo 5:31
Efe 1:7
Ebr 7:25
1Pe 2:24

d Isa 7:14

e Isa 8:8,10

f Lu 2:7

g Lu 2:21

SURA YA 2

h Mik 5:2
Lu 2:4

i Lu 1:5

j Mt 27:37

nyumbani, kwa sababu amepata mimba kupitia roho takatifu.^a **21** Atamzaa mwana, nawe utamwita jina Yesu,^{*b} kwa maana atawaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao."^c **22** Kwa kweli, yote hayo yalitukia ili kutimiza maneno haya yaliyosemwa na Yehova* kupitia nabii wake: **23** "Tazama! Bikira atapata mimba naye atazaa mwana, nao watamwita jina Imanueeli,"^d ambalo linapotafsiriwa linamaanisha, "Mungu Yuko Pamoja Nasi."^e

24 Ndipo Yosefu akaamka kutoka usingizini na kufanya kama alivyoambiwa na malaika wa Yehova,* akampeleka mke wake nyumbani. **25** Lakini hakufanya ngono naye mpaka alipozaa mwana,^f kisha Yosefu akamwita jina Yesu.^g

2 Baada ya Yesu kuzaliwa huko Bethlehemu^h ya Yudea katika siku za Mfalme Herode,^{*i} tazama! wanjimu[†] kutoka Mashariki walikuja Yerusalemu, **2** wakisema: "Yuko wapi yule aliyezaliwa awe mfalme wa Wayahudi?/ Kwa maana tuliiona nyota yake tulipokuwa Mashariki, nasi tumekuja kumsujudia."^{*} **3** Mfalme Herode aliposikia jambo hilo, yeye na watu wote huko Yerusalemu wakafadhaiika. **4** Akawakusanya wakuu wote wa makuhani na waandishi wa watu na kuwauliza mahali ambapo Kristo* alipaswa kuzaliwa. **5** Wakamwambia:

1:21 *Linafanana na jina la Kiebrania Yeshua, au YOSHUA, linalomaanisha "Yehova Ni Wokovu." **1:22, 24** *Angalia Nyongeza A5. **2:1** *Angalia Kamusi, uku. 2012. [†]Au "wataalamu wa nyota." **2:2** *Au "kumwinamia." **2:4** *Au "Masihi; Mtiwa-mafuta."

“Katika Bethlehemu^a ya Yudea; kwa maana nabii aliandika hivi: **6** ‘Na wewe, ewe Bethlehemu ya nchi ya Yuda, wewe si mji mdogo zaidi miongoni mwa magavana wa Yuda, kwa maana kutoka kwako atakuja kiongozi, atakayewachunga watu wangu Israeli.’”^b

7 Ndipo Herode akawaita wale wanajimu kwa siri na kuhakikisha kwa uangalifu kutoka kwao wakati ambapo ile nyota ilionekana. **8** Akawaita Bethlehemu na kuwambia: “Nendeni mkamtafute kwa uangalifu huyo mtoto, na baada ya kumpata mniletee habari, ili mimi pia niende kumsujudia.” **9** Baada ya kumsikiliza mfalme, wakaondoka, na tazama! nyota waliyokuwa wameona walipokuwa Mashariki^c ikawangoza mpaka iliposimama juu ya mahali alipokuwa yule mtoto. **10** Walipoiona ile nyota wakashangilia sana. **11** Walipoingia ndani ya nyumba wakamwona yule mtoto pamoja na Maria mama yake, wakapiga magoti na kumsujudia* mtoto. Pia, wakafungua hazina zao na kumpa yule mtoto zawadi—dhahabu, ubani, na manemane. **12** Hata hivyo, kwa sababu Mungu aliwaonya kupitia ndoto^d wasirudi kwa Herode, wakarudi nchini kwao kupitia njia nyingine.

13 Baada ya kuondoka, tazama! malaika wa Yehova* akamtokea Yosefu katika ndoto^e na kumwambia: “Simama, mchukue huyo mtoto na mama yake mkimbilie Misri, mkae huko mpaka ni-

2:11 *Au “kumwinamia.” 2:13, 15, 19
*Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 2

a Yoh 7:42

b 2Sa 5:2
Mik 5:2

c Mt 2:2

d Mt 2:22

e Mt 1:20
Mt 2:19

Safu ya 2

a Ho 11:1

b Mt 2:7

c Mwa 35:19

d Yer 31:15

e Mt 1:20

f Mt 2:12

g Mk 1:9
Lu 2:39

takapokwambia, kwa maana Herode yuko karibu kumtafuta huyo mtoto ili amuue.”

14 Basi Yosefu akaamka usiku, akamchukua Maria pamoja na yule mtoto wakaeenda Misri. **15** Wakakaa huko mpaka Herode alipokufa. Basi yakatimia maneno haya yaliyosemwa na Yehova* kupitia nabii wake: “Nikamwita mwangu atoke Misri.”^a

16 Herode alipoona ameshindwa akili na wale wanajimu, akakasirika sana, akaamuru wavulana wote huko Bethlehemu na wilaya zake zote wauawe, kuanzia umri wa miaka miwili kwenda chini, kulingana na wakati alikuwa amehakikisha kwa uangalifu kutoka kwa wale wanajimu.^b **17** Ndipo yakatimia maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii Yereemia: **18** “Sauti ilisikika kule Rama, kilio na kuomboleza kwingi. Raheli^c akiwalilia watoto wake, naye hakutaka kufarijiwa, kwa sababu hawako tena.”^d

19 Herode alipokufa, tazama! malaika wa Yehova* akamtokea Yosefu katika ndoto^e huko Misri **20** akamwambia: “Simama, umchukue mtoto na mama yake, nanyi mrudi katika nchi ya Israeli, kwa sababu wale waliotaka kumuua* mtoto wamekufa.” **21** Basi akaamka akamchukua mtoto na mama yake, wakarudi katika nchi ya Israeli. **22** Lakin aliposikia kwamba Arkelao alikuwa akitawala Yudea baada ya Herode baba yake, akaogopa kwenda huko. Zaidi ya hayo, alionywa na Mungu kupitia ndoto,^f basi akaenda katika eneo la Galilaya.^g

2:20 *Au “wakiitafuta nafsi ya.”

23 Akaenda kuishi katika jiji liitwalo Nazareti,^a ili kutimiza maneno haya yaliyosemwa kupitia manabii: "Ataitwa Mna-zareti."^b

3 Siku hizo Yohana^c Mbatizaji alikuja kuhubiri^d katika nyika ya Yudea, **2** akisema: "Tubuni, kwa maana Ufalme wa mbinguni umekaribia."^e **3** Kwa kweli, huyu ndiye anayezungumziwa kupitia nabii Isaya^f kwa maneno haya: "Kuna mtu anayepaza sauti nyikani: 'Tayarisheni njia ya Yehova!* Nyoosheni barabara zake.'^g **4** Yohana alivaa mavazi yaliyofumwa kwa manyoya ya ngamia na alijifunga mshipi wa ngozi kiunoni.^h Chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwituni.ⁱ **5** Basi watu kutoka Yerusalemu na Yudea yote na maeneo yote yaliyokuwa karibu na Yordani walikuwa wakimwenda,^j **6** naye akawatibiza* katika Mto Yordani,^k nao wakaungama dhambi zao waziwazi.

7 Alipoona Mafarisayo na Masadukayo^l wengi waki-ja kwenye ubatizo, akawaambia: "Enyi uzao wa nyoka,^m ni nani amewaonya ili mkimbie ghadhabu inayokuja?ⁿ **8** Basi zaeni matunda yana-yoonyesha toba. **9** Msithubutu kujiambia, 'Abrahamu ndiye baba yetu.'^o Kwa maana ninawaambia, Mungu anaweza kumwinulia Abrahamu watoto kutoka kwenye mawe haya. **10** Tayari shoka lime-wekwa kwenye mzizi wa miti.

2:23 *Inaelekea ni kutokana na neno la Kiebrania "chipukizi." 3:3 *Angalia Nyongeza A5. 3:6 *Au "akawatumbukiza; akawazamisha." 3:7 *Au "nyokavipiri."

SURA YA 2

a Yoh 1:45
b Isa 11:1
Isa 53:2
Yer 23:5
Zek 3:8

SURA YA 3

c Yoh 1:6
d Mk 1:3, 4
Lu 3:3-6
e Mt 4:17
f Mk 1:2
Yoh 1:23
g Isa 40:3
h 2Fa 1:8
i Mk 1:6
j Mk 1:5
k Mk 1:9
l Mk 12:18
Lu 7:30
m Mt 12:34
n Mt 23:33
Lu 3:7-9
Lu 21:23
o Yoh 8:33, 39

Safu ya 2

a Mt 7:19
Lu 13:6-9
b Mdo 19:4
c Yoh 1:15, 27
d Mk 1:7, 8
Yoh 1:33
Mdo 2:1, 4
1Ko 12:13
e Lu 3:16, 17
f Mal 4:1
g Mk 1:9
h Lu 3:21
i Isa 11:2
Mk 1:10, 11
Lu 4:18
Yoh 1:32
j Yoh 12:28
k Zb 2:7
Lu 9:35
l Isa 42:1
Mt 17:5
Lu 3:22

SURA YA 4

m Ebr 4:15
n Mk 1:12, 13
Lu 4:1-4
o 1Th 3:5

Basi, kila mti usiozaa matunda mazuri utakatwa na kutupwa motoni.^a **11** Mimi ninawabatiza kwa maji kwa sababu mmetubu,^b lakini yule anayekuja baada yangu ana nguvu kuliko mimi, nami si-stahili kuvivua viatu vyake.^c Yeye atawabatiza ninyi kwa roho takatifu^d na kwa moto.^e **12** Sepetu yake ya kupepetea imo mkononi mwake, naye atausafisha kabisa uwanja wake wa kupuria, na kukusanya ngano yake katika ghalla, lakini atayateketeza makapi kwa moto^f usioweza kuzimwa."

13 Ndipo Yesu akatoka Galilaya na kwenda Yordani ili abatizwe na Yohana.^g **14** Lakini Yohana akajaribu kumzuia, akisema: "Mimi ndiye ninayehitaji kubatizwa na wewe, nawe unakuja kwangu?" **15** Yesu akamjibu: "Acha iwe hivyo wakati huu, kwa maana kwa njia hiyo inafaa tufanye yote yaliyo ya uadilifu." Ndipo Yohana akaacha kumzuia. **16** Baada ya kubatizwa, mara moja Yesu akainuka kutoka katika maji; na tazama! mbingu zikafunguliwa,^h naye akaona roho ya Mungu ikishuka kama njiwa, ikija juu yake.ⁱ **17** Tazama! Pia, sauti ikasikika kutoka mbinguni^j ikisema: "Huyu ni Mwangu,^k mpendwa, ambaye ni memkubali."^l

4 Ndipo Yesu akaongozwa na roho kuingia nyikani ili akajaribiwe^m na Ibilisi.ⁿ **2** Baada ya kufunga kwa siku 40, mchana na usiku, akahisi njaa. **3** Naye Mjaribu^o akaja na kumwambia: "Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, yaambie mawe haya yawe mikate."

4 Lakini akajibu: "Imeandikwa: 'Mwanadamu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Yehova.'"*^a

5 Ndipo Ibilisi akampeleka kwenye lile jiji takatifu,^b akamsimamisha juu ya mnara* wa hekalu^c 6 na kumwambia: "Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, jitupe chini, kwa maana imeandikwa: 'Atawaagiza malaika zake kukuhusu wewe,' nao 'Watakubeba mikononi mwao, ili mguu wako usigonge jiwe.'"^d 7 Yesu akamwambia: "Tena imeandikwa: 'Usimjarihu Yehova* Mungu wako.'"^e

8 Tena Ibilisi akampeleka Yesu kwenye mlima mrefu sana, akamwonyesha falme zote za ulimwengu na utukufu wazo.^f 9 Naye akamwambia: "Nitakupa vitu hivi vyote ukianguka chini na kunifanyia tendo la ibada." 10 Ndipo Yesu akamwambia: "Nenda zako, Shetani! Kwa maana imeandikwa: 'Yehova* Mungu wako ndiye unayepaswa kumwabudu,^g na yeye peke yake ndiye unayepaswa kumtolea utumishi mtakatifu.'"^h 11 Ndipo Ibilisi akamwacha,ⁱ na tazama! malaika wakaja na kuanza kumhudumia.^j

12 Yesu aliposikia kwaomba Yohana alikuwa amekamatwa,^k akaenda Galilaya.^l

13 Isitoshe, baada ya kuondoka Nazareti, akaenda kukaa Kapernaumu^m kando ya bahari katika wilaya za Zabuloni na Naftali, 14 ili kutimiza maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii Isaya, aliyese-

4:4, 7, 10 *Angalia Nyongeza A5. 4:5

^aAu "ukuta wa ukingoni; sehemu ya juu zaidi."

SURA YA 4

a Kum 8:3

Lu 4:4

Yoh 4:34

b Ne 11:1

Isa 52:1

c Lu 4:9-12

d Zb 91:11,12

e Kum 6:16

Lu 4:12

IKo 10:9

f Lu 4:5-8

g Ufu 22:9

h Kum 6:13

Kum 10:20

Lu 4:8

i Lu 4:13

Yak 4:7

j Lu 22:43

Ebr 1:7,14

k Mk 6:17,18

Kum 3:19,20

l Mk 1:14

Lu 4:14

m Lu 4:31

Safu ya 2

a Yoh 1:9

b Isa 9:1,2

c Mt 10:7

Mk 1:14,15

d Yoh 1:42

e Mk 1:16-18

f Lu 5:10,11

g Mk 10:28

Lu 18:28

h Mt 10:2

Mt 27:55,56

Mk 3:17

Mk 10:35

Yoh 21:2

i Mk 1:19,20

j Mt 9:35

Mk 1:39

Mk 6:6

k Lu 4:16

Mdo 13:13,14

l Lu 9:11

Mdo 10:37,38

m Mk 6:55

n Mk 1:32

Mdo 5:16

o Mt 17:15

ma: 15 "Ewe nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, kando ya barabara ya bahari, ng'ambo ya Yordani, katika Galilaya ya mataifa! 16 Watu wanaokaa katika giza waliona nuru kuu, na wale wanaokaa katika eneo la kivuli cha kifo, nuru^a iliwaangazia."^b 17 Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri na kusema: "Tubuni, kwa maana Ufalme wa mbinguni umekaribia."^c

18 Alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya aliwaona ndugu wawili, Simoni, anayetwa Petro,^d na Andrea ndugu yake, wakishusha wavu baharini, kwa maana walikuwa wavuvi.^e 19 Aka-waambia: "Nifuateni, nami nitawafanya muwe wavuvi wa watu."^f 20 Mara moja waka-ziacha nyavu zao na kumfuata.^g 21 Alipoenda mbele kidogo akawaona ndugu wengine wawili, Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo.^h Walikuwa kwenye mashua pamoja na baba yao Zebedayo wakite-ngeneza nyavu zao, naye akawa-ita.ⁱ 22 Mara moja wakaa-cha ile mashua na baba yao, wakamfuata.

23 Kisha akaenda katika Galilaya yote,^j akifundisha katika masinagogi^k yao na kuhubiri habari njema ya Ufalme na kuwaponya watu kila aina ya ugonjwa na kila aina ya udhaifu.^l 24 Na habari kuhusu zikaenea katika Siria yote, nao wakamletea wote waliokuwa na magonjwa mbalimbali na walioteseka,^m wenyewe roho waovuⁿ na wenye kifafa^o na watu waliopooza, naye akawaponya. 25 Kwa hiyo, umati mkubwa ukamfua-

ta kutoka Galilaya, Dekapoli,* Yerusalemu, Yudea, na ng'ambo ya Yordani.

5 Alipouona umati, akapanda mlimani; na baada ya kuketi wanafunzi wake wakamjia. **2** Kisha akafungua kinywa chake akaanza kuwafundisha, akisema:

3 "Wenye furaha ni wale wanaotambua uhitaji wao wa kiroho,*^a kwa kuwa Ufalme wa mbinguni ni wao.

4 "Wenye furaha ni wale wanaoambleza, kwa kuwa watafarijiwa.^b

5 "Wenye furaha ni wale walio wapole,^c kwa kuwa watairithi dunia.^d

6 "Wenye furaha ni wale walio na njaa na kiu^e ya uadilifu, kwa kuwa watashibishwa.*^f

7 "Wenye furaha ni wale wenye rehema,^g kwa kuwa wataonyeshwa rehema.

8 "Wenye furaha ni wale walio safi moyoni,^h kwa kuwa watamwona Mungu.

9 "Wenye furaha ni wale wanaofanya amani,ⁱ kwa kuwa wataitwa wana wa Mungu.

10 "Wenye furaha ni wale ambao wametewa kwa ajili ya uadilifu,^j kwa kuwa Ufalme wa mbinguni ni wao.

11 "Wenye furaha ni ninyi, watu wanapowashutumua^k na kuwatesa^l na kuwasingizia kila aina ya uovu kwa sababu yangu.^m **12** Furahini na kushangilia sana,ⁿ kwa kuwa thwabu^o yenu ni kubwa mbinguni, kwa maana hivyo ndi-

4:25 *Au "Eneo lenye Majiji Kumi." 5:3 *Au "walio na kiu au njaa ya kiroho; ombaomba wa kiroho." 5:6 *Au "wataotoshelezwa."

SURA YA 5

a Lu 6:20

b Isa 61:2, 3
Mt 11:28c ITi 6:11
Tit 3:2

d Zb 37:11

e Isa 55:1
Lu 6:21

f Yoh 6:35

g Mt 6:14
Mt 18:33
Yak 2:13h Zb 24:3, 4
Zb 73:1i Ro 12:18
Ebr 12:14
Yak 3:18j Mk 10:29, 30
1Pe 3:14

k Mt 10:22

l Yoh 15:20

m Lu 6:22, 23
Yak 1:2
1Pe 4:14n Mdo 5:41
Ro 5:3

o Ebr 11:6

Safu ya 2

a 2Nya 36:16
Mdo 7:52
Ebr 11:32, 37

b Mk 9:50

c Lu 14:34, 35

d Yoh 8:12
Yoh 12:36
Flp 2:15e Mk 4:21
Lu 11:33f Efe 5:8
Flp 2:15

g Efe 5:9

h Yoh 15:8
1Pe 2:9, 12

i Lu 4:21

j Isa 40:8
Lu 16:17k Mt 15:7-9
Mt 23:23
Lu 11:42l Mt 18:3
Yoh 3:5m Mwa 9:6
Kut 20:13
Kum 5:17

vyo walivyowatesa manabii waliokuwapo kabla yenu.^a

13 "Ninyi ndio chumvi ya dunia, lakini chumvi^b ikipoteza nguvu yake, ladha yake itarudishwaje? Haifai tena, inapaswa kutupwa nje^c na kukanyagwa-kanyagwa na watu.

14 "Ninyi ndio nuru ya ulimwengu.^d Jiji lililo mlimani haliwezi kufichwa. **15** Watu hawawashi taa na kuiweka chini ya kikapu* bali huiweka kwenye kinara cha taa ili iwaangazie wote walio ndani ya nyumba.^e **16** Vivyo hivyo, acheni nuru yenu iangaze mbele ya watu,^f ili waone matendo yenu mema^g na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni.^h

17 "Msifikiri nilikuja kuharibu Sheria au Manabii. Sikuja kuharibu, bali kutimiza.ⁱ

18 Kwa kweli ninawaambia ni rahisi zaidi kwa mbingu na dunia kupitilia mbali, kuliko herufi moja iliyo ndogo zaidi au sehemu yoyote ya herufi kuondolewa katika Sheria mpaka mambo yote yatimie.^j

19 Kwa hiyo, yeyote anayevunja mojawapo ya amri hizi ndogo na kufundisha wengine kufanya hivyo, ataitwa mdogo kuhusiana na Ufalme wa mbinguni. Lakini yeyote anayeshika na kufundisha amri hizi ataitwa mkubwa kuhusiana na Ufalme wa mbinguni.

20 Kwa maana ninawaambia ikiwa uadilifu wenu hauzidi ule wa waandishi na Mafarisayo,^k hamtaingia kamwe katika Ufalme wa mbinguni.^l

21 "Mlisikia kwamba zamani watu waliambiwa: 'Usiue,^m

5:15 *Au "kikapu cha kupimia."

lakini yeyote anayeuatawajibika mahakamani.^a **22** Hata hivyo, ninawaambia kila mtu anayeendelea kumkasirikia^b ndugu yake atawajibika mahakamani; na yeyote anayemtukana ndugu yake kwa neno la dharau atawajibika katika Mahakama Kuu; na yeyote anayesema, 'Wewe mpumbavu usiyefaa kitu!' atastahili moto wa Gehena.*^c

23 "Basi, ikiwa unaleta zawadi yako kwenye madhabahu^d na hapo unakumbuka kwamba ndugu yako ana jambo fulani dhidi yako, **24** iache zawadi yako hapo mbele ya madhabahu, uende zake. Kwanza fanya amani na ndugu yako, kisha urudi na kutoa zawadi yako.^e

25 "Suluhisha mambo upesi na mtu anayekushtaki, ukiwa naye njiani kwenda mahakamani, ili asikupeleke kwa hakimu, naye hakimu kwa mtumishi wa mahakama, nawe utupwe gerezani.^f **26** Hakika ninakuambia hutatoka humo mpaka utakapolipa sarafu yako ndogo ya mwisho.*

27 "Mlisikia kwamba ilisemwa: 'Usifanye uzinzi.'^g **28** Lakini ninawaambia kila mtu anayeendelea kumtamama mwanamke^h na kumtamama tayari amefanya uzinzi naye moyoniⁱ mwake. **29** Basi, ikiwa jicho lako la kulia linafanya ujikwae, ling'oe na kulitupilia mbali.^j Kwa maana ni afadhali upoteze kiungo kimoja kuliko mwili wako wote utupwe katika Gehena.*^k **30** Pia, ikiwa

5:22 *Mahali pa kuteketezea takataka nje ya Yerusalemu. Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:26 *Tnn., "kwadrani ya mwisho." Angalia Nyongeza B14. 5:29, 30 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 5

a Law 24:17
Kum 17:8, 9

b Kol 3:8
Yak 1:19

c Mt 10:28
Lu 12:5
1Yo 3:15

d Kum 16:16

e 1Yo 4:20

f Lu 12:58, 59

g Kut 20:14
Kum 5:18
Lu 18:20
Ro 13:9

h 2Sa 11:2
Ayu 31:1

i Mk 7:20-22

j Lu 11:34

k Mt 18:9
Mk 9:47

Safu ya 2

a Kol 3:5

b Mt 18:8

c Kum 24:1
Mt 19:3, 8
Mk 10:2, 4

d Mt 19:9
Mk 10:11, 12
Lu 16:18
Ro 7:3

e Law 19:12

f Hes 30:2
Kum 23:21
Mhu 5:4

g Yak 5:12

h Isa 66:1

i Zb 48:2

j Yak 5:12

k Yoh 8:44

l Kut 21:24, 25
Law 24:20
Kum 19:21

m Met 24:29
Isa 50:6
Lu 6:29
Ro 12:17
1Pe 2:23

mkono wako wa kulia unaku-fanya ujikwae, ukate na kuu-tupilia mbali.^a Kwa maana ni afadhali upoteze kiungo kimoja kuliko mwili wako wote utupwe katika Gehena.*^b

31 "Zaidi ya hayo, ilisemwa: 'Yeyote anayemtaliki mke wake, anapaswa kumpa cheti cha talaka.'^c **32** Hata hivyo, ninawaambia kila mtu anayemtaliki mke wake kwa sababu nyingine isipokuwa uasherati,* anamweka katika kishawishi cha kufanya uzinzi, na yeyote anayemwoa mwanamke aliyetalikiwa anafanya uzinzi.^d

33 "Tena mlisikia kwamba zamani watu waliambiwa: 'Usikose kutimiza kiapo chako,^e unapaswa kutimiza nadhiri zako kwa Yehova.'^f

34 Hata hivyo, ninawaambia: Msiape kamwe^g kwa mbingu kwa sababu ni kiti cha ufalme cha Mungu; **35** wala kwa dunia kwa sababu ni mahali pake pa kuwekea miguu;^h wala kwa Yerusalemu kwa sababu ni jiji la Mfalme mkuu.ⁱ **36** Usiape kwa kichwa chako kwa sababu huwezi kugeuza unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi. **37** Acheni 'Ndiyo' yenu imaanishe ndiyo, na 'Siyo' yenu, siyo,^j kwa maana linalozidi hayo linatoka kwa yule mwovu.^k

38 "Mlisikia kwamba ilisemwa: 'Jicho kwa jicho na jino kwa jino.'^l **39** Hata hivyo, ninawaambia: Msimzuie mtu mwovu, bali yeyote anayekupiga kofi kwenye shavu la kulia, mgeuzie pia shavu la kushoto.^m **40** Na ikiwa mtu anataka kukupeleka mahaka-

5:32 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:33 *Angalia Nyongeza A5.

mani ili alichukue vazi lako la ndani, mwachie pia vazi lako la nje;^a **41** na mtu mwenye mamlaka akikulazimisha uingie katika utumishi wa kilomita moja,* nenda naye kilomita mbili. **42** Mpe yule anayekuomba, wala usimpe kisogo yule anayetaka umkopeshe.*^b

43 "Mlisikia kwamba ilisema: 'Lazima umpende jirani yako^c na kumchukia adui yako.' **44** Hata hivyo, ninawaambia: Endeeleni kuwape nda adui zenu^d na kusali kwa ajili ya wale wanaowatesa ninyi,^e **45** ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni,^f kwa kuwa yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, na hunyesha mvua juu ya waadilifu na wasio waadilifu.^g **46** Kwa maana mkiwape nda wale wanaowapenda, mnapata thawabu gani?^h Je, wakusanya kodi hawafanyi vivyo hivyo? **47** Na mkiwasalimu ndugu zenu tu, mnafanya jambo gani lisilo la kawaida? Je, watu wa mataifa hawafanyi vivyo hivyo? **48** Basi lazima muwe wakamilifu* kama Baba yenu wa mbinguni alivyo wakamilifu.ⁱ

6 "Iweni waangalifu msionyeshe uadilifu wenu mbele ya watu ili wawaone;^j la siyyo hamtapata thawabu kutoka kwa Baba yenu aliye mbinguni. **2** Basi unapotoa zawadi za rehema,* usipige tarumbeta mbele yako kama wanavyofanya wanafiki katika masinagogi na barabara-

5:41 *Tnn., "maili moja." Angalia Nyongeza B14. 5:42 *Yaani, umkopeshe bila faida au riba. 5:48 *Au "kamili." 6:2 *Au "unapowapa maskini zawadi." Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 5

a 1Ko 6:7

b Law 25:36
Kum 23:19c Law 19:18
Mk 12:31d Met 25:21
Ro 12:20e Lu 6:27, 28
Mdo 7:60
Ro 12:14

f Efe 5:1

g Lu 6:35
Mdo 14:17

h Lu 6:32, 33

i Law 19:2
Kum 18:13
Lu 6:36
1Pe 1:16

SURA YA 6

j Mt 23:5

Safu ya 2

a Met 19:17
Mt 10:42

b Lu 18:11

c Mt 6:16
Mt 23:5

d Lu 6:12

e Lu 12:30

f Lu 11:2-4

g Kut 6:3
Zb 83:18

h Eze 36:23

i Da 2:44
Mt 6:33
Ufu 11:15j Mt 26:42
1Ti 2:4
Ufu 4:11k Zb 37:10
Lu 23:43
Mdo 24:15l Zb 37:25
Met 30:8
Mt 6:34
1Ti 6:8m Mt 18:21
Mk 11:25

ni, ili wasifiwe na watu. Kwa kweli ninawaambia, wanapata thawabu yao kikamili. **3** Lakini wewe, unapotoa zawadi za rehema, usiache mko-no wako wa kushoto ujue kile ambacho mko-no wako wa kulia unafanya, **4** ili utoe zawadi za rehema kwa siri. Naye Baba yako anayetazama akiwa mahali pa siri atakulipa.^a

5 "Pia, mnaposali msifanye kama wanafiki,^b kwa maana wanapenda kusali wakiwa wamesimama katika masinagogi na kwenye kona za barabara kuu ili watu wawaone.^c Kwa kweli ninawaambia, wanapata thawabu yao kikamili. **6** Lakini unaposali, ingia ndani ya chumba chako faraghani, baada ya kufunga mlango wako, sali kwa Baba yako aliye mahali pa siri.^d Naye Baba yako anayetazama akiwa mahali pa siri atakulipa. **7** Mnaposali msiseme mambo yaleyale tena na tena, kama vile watu wa mataifa wanavyofanya, kwa maana wao hufikiri watasikiwa kwa kutumia maneno mengi. **8** Kwa hiyo, msiwe kama wao, kwa sababu Baba yenu anajua kile mna-chohitaji^e hata kabla hamjamwomba.

9 "Basi, salini hivi:^f

"Baba yetu uliye mbinguni, jina lako^g na litakaswe.*^h **10** Ufalme wakoⁱ na uje. Mapeenzi yako^j na yatendeke duniani^k kama ilivyo mbinguni. **11** Utupatie leo mkate wetu kwa ajili ya siku hii;^l **12** na utusamehe madeni yetu, kama vile tunavyowasamehe wadeni wetu.^m **13** Na usituingize

6:9 *Au "litukuzwe; lionwe kuwa takatifu."

katika majaribu,^a bali utukomboe* kutoka kwa yule mwovu.^b

14 “Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi pia;^c **15** lakini msipowasamehe watu makosa yao, naye Baba yenu hatawasamehe makosa yenu.^d

16 “Mnapofunga,^e msiwe na nyuso zenye huzuni kama wanafiki, kwa maana wao hukunja nyuso zao* ili watu waone kwamba wanafunga.^f Kwa kweli ninawaambia, wana-pata thawabu yao kikamili. **17** Lakini wewe unapofunga, paka kichwa chako mafuta na unawe uso, **18** ili usionekane kwamba unafunga kwa wanadamu bali kwa Baba yako aliye mahali pa siri. Naye Baba yako anayeona akiwa mahali pa siri atakulipa.

19 “Acheni kujiwekea hazina duniani,^g ambako nondo* na kutu hula na ambako wezi huvunja na kuiba. **20** Bada-la yake, jiwekeeni hazina mbinguni,^h ambako hazitaliwa na nondo* wala kutu,ⁱ na ambako wezi hawatavunja na kuiba. **21** Kwa maana mahali ilipo hazina yako, ndipo moyo wako utakapokuwa pia.

22 “Taa ya mwili ni jicho.^j Basi, ikiwa jicho lako linakazia jambo hususa,* mwili wako wote utakuwa mwangavu.[#] **23** Lakini ikiwa jicho lako lina wivu,^{*k} mwili wako wote utakuwa na giza. Ikiwa nuru iliyo ndani yako

6:13 *Au “utuokoe.” 6:16 *Au “hawatunzi sura au mwonekano wao.” 6:19, 20 *Aina ya wadudu. 6:22 *Au “linao-na vizuri.” Tnn., “ni rahisi.” #Au “utajawa na nuru.” 6:23 *Tnn., “ni bovu; lina uovu.”

SURA YA 6

a Mt 26:41
1Ko 10:13
Ufu 3:10

b Yoh 17:15
1Yo 5:19

c Efe 4:32
Kol 3:13

d Mt 18:35
Yak 2:13

e Mdo 13:2, 3
Mdo 14:23

f Isa 58:5
Lu 18:11, 12

g Mt 13:22
Lu 12:20
Yak 5:3

h Mt 19:21
Mk 10:21
Lu 12:33, 34
Lu 18:22

i 1Pe 1:3, 4

j Met 4:25
Lu 11:34
Efe 1:18

k Mt 20:15

Safu ya 2

a Yak 4:4

b Mt 13:22
Lu 16:13

c Zb 55:22
Flp 4:6
1Pe 5:6, 7

d 1Ti 6:8
Ebr 13:5

e Lu 12:22-28

f Ayu 38:41
Zb 147:9
Mt 10:29

g Zb 39:5

h 1Fa 10:4, 5

i Lu 10:41

j Lu 12:29-31

kwa kweli ni giza, basi giza hilo ni kubwa sana!

24 “Hakuna anayeweza kutatumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia mmoja na kumpenda mwingine,^a au atashikamana na mmoja na kumdharau mwingine. Hamwezi kutumikia Mungu na Utajiri.^b

25 “Kwa hiyo ninawaambia: Acheni kuhangaikia^c uhai wenu* kuhusu kile mtakachokula au kunywa, au juu ya miili yenu kuhusu kile mtakachovaa.^d Je, uhai[#] si zaidi ya chakula na mwili zaidi ya mavazi?^e **26** Waangalieni kwa makini ndege wa angani;^f hawapandi mbegu, hawavuni, wala kukusanya ghalani, na bado Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, ninyi si wenye thamani kuliko wao?

27 Ni nani kati yenu ambaye kwa kuhangaika anaweza kurefusha uhai wake kwa mkono

mmoja?^{*g} **28** Pia, kwa nini mnahangaika kuhusu mavazi? Jifunzeni kutoka kwa mayungiyungi* ya shambani, jinsi yanavyokua; hayafanyi kazi, wala hayasokoti; **29** lakini ninawaambia hata Sulemani^h katika utukufu wake wote hakupambwa kama maua hayo.

30 Basi, ikiwa Mungu huivika hivyo mimea ya shambani, ambayo ipo hapa leo na kesho hutupwa ndani ya jiko, je, hatawavika vizuri zaidi ninyi wenye imani ndogo? **31** Kwa hiyo msihangaika^e kamwe na kusema, ‘Tutakula nini?’ au, ‘Tutakunywa nini?’ au, ‘Tutatawa nini?’ **32** Kwa maana yanatafuta vitu hivi

6:25 *Au “nafsi zenu.” #Au “nafsi.” 6:27 *Angalia Nyongeza B14. 6:28 *Aina ya maua.

vyote kwa bidii. Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mnahitaji vitu hivi vyote.

33 "Basi, endeleeni kuatafuta kwanza Ufalme na uadilifu wake,* nanyi mtaongeze-wa hivi vitu vingine vyote.^a

34 Basi, msihangaikwa kama kuhusu kesho,^b kwa maana kesho itakuwa na mahangai-ko yake yenyewe. Kila siku ina matatizo yake ya kutosha.

7 "Acheni kuhukumu^c ili msihukumiwe; **2** kwa maana kwa hukumu mnayohukumu, mtahukumiwa,^d na kwa kipimo mnachowapimia watu, ndicho watawachowapimia.^e

3 Basi, kwa nini unautazama unyasi ulio katika jicho la ndugu yako lakini huoni boriti lililo katika jicho lako mwenyewe?^f

4 Au unawezaje kumwambia ndugu yako, 'Niruhusu niutoe unyasi ulio katika jicho lako,' na huku tazama! una boriti katika jicho lako? **5** Mnafiki! Kwanza toa boriti katika jicho lako, kisha utaona vizuri jinsi ya kuutoa unyasi katika jicho la ndugu yako.

6 "Msiwape mbwa kitu kitakatifu, wala msiwatupie nguruwe lulu zenu,^g wasije wakazikanyaga-kanyaga chini ya miguu yao, kisha wageuke na kuwararua ninyi.

7 "Endeleeni kuomba, nanyi mtapewa;^h endeleeni kutafuta, nanyi mtapata; endeleeni kupiga hodi, nanyi mtafunguliwa;ⁱ **8** kwa maana kila mtu anayeomba hupokea,^j na kila mtu anayetafuta hupata, na kila mtu anayepiga hodi, atafunguliwa. **9** Kwa kweli, ni nani miongoni mwenu ambaye mwanawe

SURA YA 6

a Zb 37:25

b Kut 16:4, 19

SURA YA 7

c Lu 6:37

Ro 2:1

Ro 14:13

d Mt 18:33, 34

Yak 2:13

e Mk 4:24

Lu 6:38

Gal 6:7

f Lu 6:41, 42

g Met 9:7

Mt 10:14

h Mk 11:24

Yak 1:5

1Yo 5:14

i Lu 11:9-13

j Yoh 14:13

1Yo 3:22

Safu ya 2

a Yak 1:17

b Lu 11:13

c Lu 6:31

d Ro 13:10

Gal 5:14

e Lu 13:24

f Mdo 14:22

1Pe 4:18

g Mt 24:11

2Pe 2:1

1Yo 4:1

h Lu 6:26

i Mdo 20:29, 30

j Lu 6:44

k Mt 12:33

l Lu 6:43

m Mt 3:10

Lu 13:6, 9

n Mt 12:33

akimwomba mkate, atampa jiwe? **10** Au akimwomba samaki, je, atampa nyoka? **11** Kwa hiyo, ingawa ninyi ni waovu, mnajua jinsi ya kuwapa watoto wenu zawadi nzuri, je, Baba yenu aliye mbinguni hatawapa hata zaidi vitu vye-ma^a wale wanaomwomba?^b

12 "Basi, mambo yote mna-yotaka watu wawatendee ni-nyi, lazima ninyi pia mwatendee vivyo hivyo.^c Kwa kweli, hiyo ndiyo maana ya Sheria na Manabii.^d

13 "Ingieni kupitia lango jembamba,^e kwa sababu lango ni pana, na barabara inayoongoza kwenye uharibifu ina nafasi kubwa, na ni wengi wanaoipitia; **14** lakini lango ni jembamba na barabara inayoongoza kwenye uzima ina nafasi ndogo, na ni wachache wanaoipata.^f

15 "Jihadharini na manabii wa uwongo^g ambao huja kweni katika mavazi ya kondoo,^h lakini ndani wao ni mbwamwitu wakali.ⁱ **16** Kwa matunda yao mtawatambua. Je, watu huchuma zabibu kwenye miiba au tini kwenye michongoma?^j **17** Vivyo hivyo, kila mti mzuri huzaa matunda mazuri, lakini kila mti uliooza huzaa matunda mabaya.^k **18** Mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti uliooza hauwezi kuzaa matunda mazuri.^l **19** Kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa ndani ya moto.^m

20 Kwa kweli, mtawatambua watu hao kwa matunda yao.ⁿ **21** "Si kila mtu anayenia-mbia, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika Ufalme wa mbinguni, bali yule anayefanya

mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni ndiye atakayeingia.^a

22 Wengi wataniambia siku hiyo: ‘Bwana, Bwana,^b je, hatukutoa unabii katika jina lako, na kufukuza roho waovu katika jina lako, na kufanya matendo mengi yenye nguvu katika jina lako?’^c **23** Ndipo nitakapowaambia: ‘Sikuwajua ninyi kama! Ondokeni kwangu, ninyi mnaotenda uasi sheria!’^d

24 “Kwa hiyo, kila mtu anayesikia haya maneno yangu na kuyatenda ni kama mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake kwenye mwamba.”^e **25** Kisha mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, upepo ukavuma na kuipiga nyumba hiyo, lakini haikuporomoka, kwa maana msingi wake ulikuwa umejengwa kwenye mwamba. **26** Zaidi ya hayo, kila mtu anayesikia haya maneno yangu lakini hayatendi ni kama mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba juu ya mchanga.^f **27** Kisha mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, upepo ukavuma na kuipiga nyumba hiyo,^g nayo ikaporomoka na kuharibika kabisa.”

28 Yesu alipomaliza kusema maneno hayo, umati ukashangazwa na njia yake ya kufundisha,^h **29** kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye mamlaka,ⁱ na si kama waandishi wao.

8 Yesu aliposhuka kutoa ka mlimani, umati mku-bwa ukamfuata. **2** Na tazama! mtu fulani mwenye ukoma akaja na kumsujudia* aki-mwambia: “Bwana, ikiwa tu unataka, unaweza kunitaka-

SURA YA 7

a Ro 2:13
Yak 1:22
1Yo 2:17
1Yo 5:3

b Lu 6:46

c Yer 14:14
Yer 27:15

d Lu 13:25-27

e Lu 6:47-49
Yak 1:25

f Yak 1:23, 24

g 1Ko 3:13

h Mk 1:22
Lu 4:32

i Yoh 7:46

Safu ya 2

SURA YA 8

a Mk 1:40-44
Lu 5:12-14

b Mk 1:41
Lu 5:13

c Isa 53:4

d Mt 9:30
Mt 12:15, 16
Mk 7:35, 36

e Law 14:2
Lu 17:14

f Law 14:3, 4
Law 14:19, 20

g Lu 7:1-9

h Mt 15:28
Lu 7:9

i Lu 13:29

j Lu 13:28

k Mt 9:29
Mt 15:28
Mk 9:23

l Lu 7:10

sa.”^a **3** Basi akaunyoosha mkono wake, akamgusa na kusema: “Ninataka! Takasika.”^b Mara moja ukoma wake ukatakasika.^c **4** Kisha Yesu akamwambia: “Usimwambie mtu yeyote,^d bali nenda, ukajionyeshe kwa kuhani,^e na utoe zawadi ambayo Musa aliagiza,^f ili kuwa ushahidi kwao.”

5 Alipoingia Kapernaumu, ofisa mmoja wa jeshi alimjia, akamsihi^g **6** na kusema: “Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani na ana ugonjwa wa kupooza, naye anateseka sana.” **7** Akamwambia: “Nikifika huko, nita-mponya.” **8** Ofisa huyo akamjibu: “Bwana, sistahili uingie ndani ya nyumba yangu, lakini sema tu neno na mtumishi wangu atapona. **9** Kwa maana mimi pia niko chini ya mamlaka, na nina wanajeshi walio chini yangu, nami humwambia mmoja, ‘Nenda!’ naye huenda, na mwingine, ‘Njoo!’ naye huja, na mtumwala wangu, ‘Fanya hili!’ naye hulifanya.” **10** Yesu aliposikia hayo, akashangaa na kuwaambia wale waliomfuata: “Ninawaambia ukweli, si-jaona mtu yeyote katika Israeli mwenye imani kubwa kama hii.^h **11** Lakini ninawaambia kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi na kuketi mezani pamoja na Abrahamu, Isaka, na Yakobo katika Ufalme wa mbinguni;ⁱ **12** lakini wana wa Ufalme watatupwa nje gizani. Huko ndiko watalia na kusa-ga meno yao.”^j **13** Kisha Yesu akamwambia yule ofisa wa jeshi: “Nenda. Na iwe kama ulivyoamini.”^k Na yule mtumishi akapona saa ileile.^l

14 Yesu alipoingia nyumbani kwa Petro, alimwona mama mkwe wa Petro^a akiwa amelala akiugua homa.^b

15 Basi Yesu akamgusa mkononi,^c naye akapona homa, akasimama na kuanza kumhudumia. **16** Lakini ilipofika jioni, watu walimletea watu wengi wenye roho waovu; akawafukuza hao roho kwa kusema neno moja, naye akawaponya wote waliokuwa wakite-seka, **17** ili yatimie maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii Isaya: “Yeye mwenyewe aliyachukua magonjwa yetu na kuyacheba maradhi yetu.”^d

18 Yesu alipoona umati umemzunguka, akaagiza wawuke kwenda ng’ambo ya bahari.^e **19** Mwandishi fulani akaja na kumwambia: “Mwalimu, nitakufuata popote utakapoenda.”^f **20** Lakini Yesu akamwambia: “Mbewe ha wana mapango na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa binadamu hana mahali pa kulaza kichwa chake.”^g **21** Kisha mwanafunzi mwingine akamwambia: “Bwana, ni-ruhusu kwanza niende nikamzike baba yangu.”^h **22** Yesu akamwambia: “Endelea kuni-fuata, waache wafu wawazike wafu wao.”ⁱ

23 Alipopanda kwenye mashua, wanafunzi wake wakamfuata.^j **24** Na tazama! dhoruba kubwa ikatokea baharini, hata mawimbi yakaa-nza kuifunika mashua; lakini Yesu alikuwa amelala usingizi.^k **25** Wakaja na kumwamsha wakisema: “Bwana, tuokoe, tuko karibu kuangamia!” **26** Lakini akawauliza: “Kwa nini mnaogopa sana, ninnye wenyewe imani ndogo?”^l Kisha aka-

SURA YA 8

a 1Ko 9:5

b Mk 1:29-34
Lu 4:38-41c Mk 5:41
Mdo 3:7

d Isa 53:4

e Mk 4:35
Lu 8:22

f Lu 9:57

g Lu 9:58
2Ko 8:9

h Lu 9:59

i Lu 9:60

j Mk 4:36

k Mk 4:37-41
Lu 8:23-25l Mt 14:31
Mk 4:40

Safu ya 2

a Zb 89:9
Zb 107:29
Lu 8:25b Mk 5:1-3
Lu 8:26, 27

c Lu 4:34, 41

d Mk 1:24
Yak 2:19e Mk 5:7-10
Lu 8:28

f Mk 5:11-17

g Kum 14:8
Lu 8:31-34

h Lu 8:35-37

SURA YA 9

i Mt 4:13
Mk 2:1

simama na kuukemea upepo na bahari, kukawa shwari kabisa.^a **27** Basi wanafunzi wakashangaa na kusema: “Huyu ni mtu wa aina gani? Hata upepo na bahari vinamtii.”

28 Alipofika upande ule mwingine na kuingia katika eneo la Wagadarene, alikutana na wanaume wawili waliokuwa na roho waovu wakitoka makaburini.^{*b} Walikuwa wakali sana, hivi kwamba hakuna mtu aliyekuwa na ujasi-ri wa kupita katika barabara hiyo. **29** Na tazama! wakapiga mayowe wakisema: “Kwa nini unatusumbua, Mwana wa Mungu?^c Je, umekuja kututesa^d kabla ya wakati uliowe-kwa?”^e **30** Lakini kule mbali nao kulikuwa na kundi la nguruwe wengi wakila.^f **31** Kwa hiyo wale roho waovu wakaa-nza kumsihi: “Ukitufukuza, turuhusu tuingie katika lile kundi la nguruwe.”^g **32** Basi akawaambia: “Nendeni!” Ndi-po wakatoka na kuingia ndani ya wale nguruwe, na tazama! kundi zima likatimua mbio, likaruka poromoko* likazama baharini na kufa maji. **33** Lakini wachungaji wakakimbia, na walipoingia jijini, wakasimulia mambo yote, kutia ndani habari kuhusu wale watu waliokuwa na roho waovu. **34** Na tazama! watu wote katika jiji hilo wakaenda kukutana na Yesu, na walipomwona, wakamsihi aondoke katika eneo lao.^h

9 Basi akapanda mashua, akavuka bahari na kwenda katika jiji lake.ⁱ **2** Na tazama! wakamletea mtu aliyepooza,

8:28 *Au “makaburi ya ukumbusho.”
8:32 *Au “ukingo wenye mteremko mkali.”

akiwa amelala kwenye kitanda.* Alipoona imani yao, Yesu akamwambia yule mtu aliyepooza: “Jipe moyo mwangu! Umesamehewa dhambi zako.”^a **3** Sasa baadhi ya waandishi wakaambiana: “Mtu huyu anakufuru.” **4** Yesu, akijua fikira zao, akasema: “Kwa nini mnawaza mambo maovu katika mioyo yenu?”^b **5** Kwa mfano, ni jambo gani rahisi zaidi kusema, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema, ‘Simama utembe?’^c **6** Hata hivyo, ili mjue kwamba Mwana wa binadamu ana mamlaka ya kusamehe dhambi duniani—” kisha akamwambia yule mtu aliyepooza: “Simama, chukua kitanda chako, uende nyumbani.”^d **7** Ndipo akasimama, akaenda nyumbani. **8** Umati ulipoona hivyo ukaogopa, nao wakamtukiza Mungu aliyewapa wanadamu mamlaka ya namna hiyo.

9 Yesu alipokuwa akiondoka mahali hapo akamwona mtu aliyelitwa Mathayo akiwa ameketi kwenye ofisi ya kodi, akamwambia: “Njoo uwe mfuasi wangu.” Mara moja akasimama na kumfuata.^e **10** Baadaye alipokuwa akila* katika nyumba, tazama! wakusanya kodi wengi na watenda dhambi wakaja na kuanza kula^f pamoja na Yesu na wanafunzi wake.^f **11** Lakini Mafarisayo walipoona hivyo wakawauliza wanafunzi wake: “Kwa nini mwalimu wenu anakula pamoja na wakusanya kodi na watenda dhambi?”^g **12** Yesu alipowasikia, akasema: “Watu wenye afya hawa-

9:2 *Au “machela.” 9:10 *Au “akiwa ameketi mezani.” #Au “kuketi mezani.”

SURA YA 9

a Mk 2:3-12
Lu 5:18-26

b Yoh 2:24, 25

c Mk 2:9

d Mk 2:10, 11
Lu 5:24
Yoh 5:8

e Mk 2:14
Lu 5:27, 28

f Mk 2:15-17
Lu 5:29-32

g Lu 7:39
Lu 15:2
Lu 19:7

Safu ya 2

a Lu 5:31

b Met 21:3
Ho 6:6
Mt 12:7

c Mk 2:18-20
Lu 5:33-35

d Mt 22:2

e Mt 26:2

f Mk 2:21, 22
Lu 5:36-39

g Mk 5:22-24
Lu 8:41, 42
Yoh 11:25

hitaji daktari, lakini wagonjwa wanamhitaji.^a **13** Nendeni, basi, mkajifunze maana ya maneno haya: ‘Ninataka rehma, si dhahibu.’^b Kwa maana sikuja kuwaita waadilifu, bali watenda dhambi.”

14 Kisha wanafunzi wa Yohana wakaja na kumuuliza: “Kwa nini sisi na Mafarisayo hufunga lakini wanafunzi wako hawafungi?”^c **15** Ndipo Yesu akawaambia: “Rafiki za bwana harusi hawahitaji kuomboleza bwana harusi^d anapokuwa pamoja nao, sivyo? Lakini siku zitakuja ambapo bwana harusi atoa ndolewa kwao,^e ndipo watakapofunga. **16** Hakuna mtu anayeshona kiraka cha kitambaa kipya juu ya vazi la nje la zamani; kwa maana hicho kitambaa kipya kitatoka kwenye hilo vazi nalo litararuka vibaya zaidi.^f **17** Wala watu hawaweiki divai mpya katika viriba vya divai vilivyochakaa. Wakifanya hivyo, viriba hivyo vitapasuka na divai itamwagika navyo viriba vitaharibika. Lakini watu huweka divai mpya katika viriba vipya vya divai, na vitu vyote viwili huhifadhiwa.”

18 Alipokuwa akiwaambia mambo hayo, tazama! mtawala fulani aliyekuwa amekaribia, akaja na kumsujudia* akisema: “Kufikia sasa binti yangu atakuwa amekufa; lakini njoo uweke mkono wako juu yake naye atakuwa hai.”^g

19 Ndipo Yesu akasimama, akamfuata pamoja na wanafunzi wake. **20** Na tazama! mwanamke aliyekuwa na mti-

9:18 *Au “kumwinamia.”

mwanamke aliyekuwa na mti-ririko wa damu^a kwa miaka 12 akaja kutoka nyuma na kugusa upindo wa vazi lake la nje,^b **21** kwa maana alikuwa aki-jiambia: “Nikigusa tu vazi lake la nje, nitapona.” **22** Yesu akageuka, na alipomwona, akamwambia: “Jipe moyo, binti yangu! Imani yako imeku-ponya.”^c Na kutoka saa hiyo, yule mwanamke akapona.^d

23 Basi alipoingia katika nyumba ya yule mtawala na kuwaona watu waliokuwa wa-kipiga filimbi na umati ulioku-wa na vurugu,^e **24** Yesu aka-sema: “Ondokeni hapa, kwa maana msichana huyu mdo-go hajafa bali amelala usingi-zi.”^f Ndipo wakaanza kumche-ka kwa dharau. **25** Mara tu umati ulipoondolewa, Yesu akaingia na kumshika mkono,^g kisha yule msichana mdogo akainuka.^h **26** Bila shaka, ha-bari hiyo ilienea katika eneo hilo lote.

27 Yesu alipokuwa akito-ka huko, wanaume wawili vi-pofuⁱ wakamfuata, wakipa-za sauti: “Tuhurumie, * Mwa-na wa Daudi.” **28** Alipoingia ndani ya nyumba, wale wa-naume vipofu wakamjia, Yesu akawauliza: “Je, mna imani kwamba ninaweza kufanya hi-vyo?”ⁱ Wakamjibu: “Ndiyo Bwana.” **29** Kisha akayagusa macho yao,^k akasema: “Na itendeke kwenu kulingana na imani yenu.” **30** Na macho yao yakaanza kuona. Zaidi ya hayo, Yesu akawaonya vika-li: “Msimwambie yeyote jambo hili.”^l **31** Lakini walipotoka nje, wakaeneza habari kumhu-su katika eneo hilo lote.

9:27 *Au “Tuonyeshe rehema.”

SURA YA 9

a Law 15:25

b Mk 5:25-34
Mk 6:56
Lu 8:43-48

c Mk 10:52
Lu 7:50
Lu 17:19
Lu 18:42

d Yoh 4:53

e Mk 5:38-43
Lu 8:52-56

f Yoh 11:11

g Mk 9:27

h Lu 8:55

i Mt 20:30

j Mdo 14:9, 10

k Mt 20:34

l Isa 42:2

Mt 12:15, 16
Mk 1:44, 45
Mk 7:35, 36

Safu ya 2

a Mt 12:22

Lu 11:14

b Mt 15:31

c Mk 2:12

d Mt 12:24

Mk 3:22

Lu 11:15

e Mt 4:23

f Mt 14:14

Ebr 4:15

g Hes 27:16, 17

1Fa 22:17

Eze 34:5

Mk 6:34

h Lu 10:2

Yoh 4:35

i Ro 10:14

SURA YA 10

j Mk 3:14, 15

Mk 6:7

Lu 9:1, 2

k Mk 3:16-19

Lu 6:13-16

Mdo 1:13

l Yoh 1:42

Mdo 15:14

m Mk 1:16

Yoh 1:40

n Mt 4:21

o Yoh 1:45

p Yoh 11:16

Yoh 20:27

q Mk 2:14

Lu 5:27

r Mt 26:47

Yoh 13:18

32 Walipokuwa wakiondo-ka, tazama! watu wakamletea bubu aliyekuwa na roho mwo-vu,^a **33** baada ya yule roho mwovu kufukuzwa, yule bubu akaongea.^b Basi, umati uk-shangaa na kusema: “Jambo kama hili halijawahi kuoneka-na katika Israeli.”^c **34** Lakini Mafarisayo walikuwa wakise-ma: “Anawafukuza roho wao-vu kwa nguvu za mtawala wa roho waovu.”^d

35 Yesu akaondoka ili kute-mbelea majiji na vijiji vyote, akifundisha katika masinago-gi yao na kuhubiri habari nje-ma ya Ufalme na kuponya kila aina ya ugonjwa na kila aina ya udhaifu.^e **36** Alipoona umati akausikitikia,^f kwa sababu wa-likuwa wamechunwa ngozi na kutupwa huku na huku kama kondoo wasio na mchungaji.^g **37** Ndipo akawaambia wana-funzi wake: “Ndiyo, mavuno ni mengi, lakini wafanyakazi ni wachache.”^h **38** Kwa hiyo, mwombeni Bwana wa mavuno awatume wafanyakazi katika mavuno yake.”ⁱ

10 Basi akawaita wanafu-nzi wake 12 na kuwapa mamlaka ya kuwafukuza roho waovu^j na kuponya kila aina ya ugonjwa na kila aina ya udhaifu.

2 Haya ndiyo majina ya wale mitume 12:^k Simoni, ai-twaye Petro,^l na Andrea^m ndu-gu yake; Yakobo na Yohanaⁿ wana wa Zebedayo; **3** Fili-po na Bartholomayo;^o Tomasi^p na Mathayo^q mkusanya kodi; Yakobo mwana wa Alfayo; na Thadayo; **4** Simoni Mkana-nayo,^{*} na Yuda Iskariote, ambaye baadaye alimsaliti.^r

10:4 *Au “mwenye bidii.”

5 Yesu akawatuma hao 12 na kuwaagiza:^a “Msiende katika barabara ya mataifa, wala msiingie katika jiji lolote la Wasamaria;^b 6 badala yake, nendeni kwa kondoo walio-potea wa nyumba ya Israeli.^c 7 Mnapoenda, hubirini mkisema: ‘Ufalme wa mbinguni ume-karibia.’^d 8 Ponyeni wago-njwa,^e fufueni wafu, takaseni wenye ukuma, fukuzeni roho waovu. Mlipokea bure, toeni bure. 9 Msichukue dhahabu, fedha, wala shaba kwenye mishi-pi yenu ya pesa,^f 10 wala mfuko wa chakula kwa ajili ya safari, wala mavazi mawili,^g wala viatu, wala fimbo,^g kwa maana mfanyakazi anastahili chakula chake.^h

11 “Mtakapoingia katika jiji au kijiji chochote, tafu-teni humo mtu anayestahili, na mkae humo mpaka mta-ka-poondoka.ⁱ 12 Mnapoi-ngia katika nyumba, wasali-muni watu wa nyumba hiyo. 13 Ikiwa nyumba hiyo inasta-hili, amani mnayoitakia na iwe juu yake;^j lakini kama haistahi-li, amani yenu na iwarudie ni-nyi. 14 Popote pale ambapo mtu hawakaribishi au kusiki-liza maneno yenu, mnapoto-ka katika nyumba hiyo au jiji hilo, kung’uteni mavumbi yali-yo kwenye miguu yenu.^k 15 Kwa kweli ninawaambia, katika Siku ya Hukumu itaku-wa afadhali zaidi kwa Sodoma na Gomora^l kuliko kwa jiji hilo.

16 “Tazama! Ninawatuma kama kondoo katikati ya mbwamwitu; kwa hiyo iweni waangalifu* kama nyoka na wasio na hatia kama njiwa.^m 17 Jihadharini na watu, kwa

10:10 *Au “vazi la ziada.” 10:16 *Au “iweni wenye kujihadhari.”

SURA YA 10

a Mk 6:7
Lu 9:1, 2
b 2Fa 17:24
c Isa 53:6
Eze 34:6
Mdo 13:45, 46
d Mt 4:17
Lu 10:9
e Lu 9:2
f Mk 6:8, 9
g Lu 9:3
h Lu 10:7
1Ko 9:7, 14
i Mk 6:10
Lu 9:4
j Lu 10:5
k Mk 6:11
Lu 9:5
Lu 10:6, 11
Mdo 13:50, 51
l Mwa 19:4, 5
2Pe 2:6
Yud 7
m Flp 2:14, 15

Safu ya 2

a Mt 24:9
b Mdo 5:40
2Ko 11:24
c Mt 23:34
Mk 13:9
Lu 21:12, 13
d Mdo 4:8
Mdo 24:10
Mdo 25:23
Mdo 26:25
Mdo 27:23, 24
e Mt 24:14
f Mk 13:11
Lu 12:11, 12
Lu 21:14, 15
g Yoh 14:26
h Mk 7:6
Mt 10:36
i Mt 24:9
Lu 21:17
Yoh 15:21
j Mt 24:13
Lu 21:19
Ufu 2:10
k Mt 23:34
Mdo 8:1
l Yoh 15:20
m 1Pe 2:21
n Mt 12:24
Mk 3:22
Lu 11:15
Yoh 8:48
o Mk 4:22
Lu 8:17

maana watawapeleka maha-kamani^a na kuwapiga mije-ledi^b katika masinagogi^c yao. 18 Nanyi mtapelekwa mbele ya magavana na wafalme^d kwa ajili yangu, ili kuwa ushahidi kwao na kwa mataifa.^e 19 Hata hivyo, mtakapope-lekwa, msihangaike kuhusu jambo mtakalosema au jinsi mtakavyolisema, kwa sababu mapewa jambo la kusema ka-tika saa hiyo;^f 20 kwa maa-na si ninyi tu mnaosema, bali ni roho ya Baba yenu inayo-sema kupitia ninyi.^g 21 Zaidi ya hayo, mtu atamtoa ndugu yake auawe, na baba ata-mtoa mtoto wake, na wato-to watainuka dhidi ya wazazi na kufanya wauawe.^h 22 Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa sababu ya jina langu,ⁱ lakini yule atakayevumilia* mpa-ka mwisho ndiye atakayeoko-lewa.^j 23 Mnapoteswa katika jiji moja, kimbilieni jiji lingi-ne;^k kwa kweli ninawaambia, hamtamaliza kamwe kuzungu-ka majiji ya Israeli kabla ya Mwana wa binadamu kufika.

24 “Mwanafunzi hamzidi mwalimu wake, wala mtu-mwa hamzidi bwana wake.^l 25 Inatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake.^m Ikiwa watu wamemwi-ta bwana wa nyumba Beel-zebubi,ⁿ namna gani watu wa nyumbani mwake? 26 Basi msiwaogope, kwa maana ha-kuna jambo lolote lililofu-nikwa ambalo halitafunuliwa, na hakuna siri yoyote ambayo haitafichuliwa.^o 27 Jambo ninalowaambia gizani, liseme-

10:22 *Au “anayevumilia.” 10:25 *Jina lingine la Shetani, mkuu, au mtawala, wa roho waovu.

ni nuruni, na jambo mnalosisikia likinong' onwa, lihubirini juu ya paa za nyumba.^a

28 Na msiwaogope wale wanaoua mwili lakini hawawezi kuuwa nafsi;^{*b} badala yake, mwogopeni yule anayeweza kuangamiza nafsi na mwili katika Gehena.^{*c} **29** Shore wawili huuzwa kwa sarafu ya thamani ndogo, * sivyo? Lakini hakuna hata mmoja wao atakayeanguka chini bila Baba yenu kujua.^d **30** Lakini hata nywele zote za vichwa vyenu zimehesabiwa. **31** Kwa hiyo msioogope; ninyi ni wenye thamani kuliko shore wengi.^e

32 "Basi kila mtu anayenikiri mbele ya watu,^f mimi pia nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni.^g **33** Lakini yeyote anayenikana mbele ya watu, mimi pia nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.^h **34** Msifikiri nilikuja kuleta amani duniani, si kuja kuleta amani, bali upanga.ⁱ **35** Kwa maana nilikuja kuleta mgawanyiko, mtu dhidi ya baba yake, binti dhidi ya mama yake, na binti mkwe dhidi ya mama mkwe wake.^j **36** Kwa kweli, adui za mtu watakuwa watu wa nyumbani mwake. **37** Yeyote anayempenda baba au mama kuliko anavyonipenda hanistahili; na yeyote anayempenda mwana au binti kuliko anavyonipenda hanistahili.^k **38** Na yeyote asiyechukua mti wake wa mateso* na kunifuata hani-stahili.^l **39** Yeyote anayeipa-

10:28 *Au "uhai," yaani, tumaini la kuishi. [#]Angalia Kamusi, uku. 2012. **10:29** *Tnn., "kwa sarafu moja ya asarioni." Angalia Nyongeza B14. **10:38** *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mti wa mateso."

SURA YA 10

- a Lu 12:3
b Met 29:25
Ufu 2:10
c Lu 12:4, 5
Ebr 10:31
d Lu 12:6, 7
e Mt 6:26
f Ro 10:9
g Lu 12:8, 9
Ufu 3:5
h Mk 8:38
Lu 9:26
2Ti 2:12
i Lu 12:51-53
j Mik 7:6
k Mt 19:29
Lu 14:26
l Mt 16:24, 25
Mk 8:34, 35
Lu 9:23
Lu 14:27

Safu ya 2

- a Lu 17:33
Yoh 12:25
b Mt 25:40
Lu 10:16
Yoh 12:44
Yoh 13:20
c 1Fa 17:9, 10
1Fa 17:20-23
2Fa 4:8
2Fa 4:13-17
d Mt 25:40
Mk 9:41
Ebr 6:10

SURA YA 11

- e Mt 4:23
Mt 19:1
Lu 9:6
f Mt 14:3
Mk 6:17
g Lu 7:18-23
h Mt 3:11
Yoh 1:15
i Lu 7:22
j Isa 35:5, 6
Isa 61:1
k Mt 8:3
l Mt 4:23
m Mk 6:3
Lu 7:23
1Ko 1:23
1Pe 2:7, 8
n Mt 3:1, 5
o Lu 7:24-28

ta nafsi yake* ataipoteza, na yeyote anayeipoteza nafsi yake* kwa ajili yangu ataipata.^a

40 "Yeyote anayewapokea ninyi ananipokea mimi pia, na yeyote anayenipokea mimi anampokea pia Yule aliyenituma.^b **41** Yeyote anayempokea nabii kwa sababu ni nabii atapata thawabu ya nabii,^c na yeyote anayempokea mtu mwadilifu kwa sababu ni mwadilifu atapata thawabu ya mtu mwadilifu. **42** Na yeyote anayempa mmoja wa hawa wadogo kikombe tu cha maji baridi ya kunywa kwa sababu ni mwanafunzi wangu, kwa kweli ninawaambia, hatapoteza kamwe thawabu yake."^d

11 Yesu alipomaliza kuwapa wanafunzi wake 12 maagizo, akaondoka huko na kwenda kufundisha na kuhubiri katika majiji yao.^e

2 Lakini Yohana akiwa jela^f alisikia mambo ambayo Kristo alikuwa akifanya, akawatuma wanafunzi wake^g **3** wamuulize: "Je, wewe ndiye Yule Anayekuja, au tumtarajie mwingine?"^h **4** Yesu akawajibu: "Nendeni mkamwambie Yohana mambo mnayosikia na kuona:ⁱ **5** Vipofu wanaona,^j viwete wanatembea, wenye ukoma^k wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.^l **6** Mwenye furaha ni mtu ambaye hapati ndani yangu sababu ya kukwaza."^m

7 Hao walipoondoka, Yesu akaanza kuuambia umati kumhusu Yohana: "Mlienda nyikani kuona nini?"ⁿ Tete likitikiswa na upepo?^o **8** Basi,

10:39 *Au "uhai wake."

mlienda kuona nini? Mtu aliyevaa mavazi laini?* Kwa maana wale wanaovaa mavazi laini wamo katika nyumba za wafalme. **9** Basi kwa kweli, kwa nini mlienda? Kumuona nabii? Ndiyo, ninawaambia, mtu aliye zaidi ya nabii.^a **10** Huyu ndiye ambaye imeandikwa hivi kumhusu: "Tazama! Ninamtuma mjumbe wangu mbele yako,* ili akutayarishie njia mbele yako!"^b **11** Kwa kweli ninawaambia, kati ya wale waliozaliwa na wanawake hajatokea mtu mkuu kuliko Yohana Mbatizaji, lakini mtu mdogo zaidi katika Ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye.^c **12** Tangu siku za Yohana Mbatizaji mpaka sasa, Ufalme wa mbinguni ndio mradi ambao watu wanajitahidi kuufikia, na wale wanaojitahidi sana wanaupata.^d **13** Kwa maana, maneno yote ya Manabii na Sheria yalitabiri hadi wakati wa Yohana;^e **14** na mkitaka kukubali, yeye ndiye 'Eliya anayepaswa kuja.'^f **15** Aliye na masikio na asikilize.

16 "Nitakifaninisha kizazi hiki na nani?"^g Ni kama watoto walioketi sokoni wakiwapazia wenzao sauti, **17** wakisema: "Tuliwapigia filimbi, lakini hamkucheza dansi; tuliomboleza, lakini hamkujipiga-piga kwa huzuni." **18** Vivyo hivyo, Yohana hakuja akila wala kunywa, lakini watu wanasema, 'Ana roho mwovu.' **19** Mwana wa binadamu alikuja akila na kunywa,^h lakini watu wanasema, "Tazama! Yeye ni mlafi na mwenye mazoea ya kunywa divai, rafiki ya wakusa-

11:8 *Au "mavazi bora." 11:10 *Tnn., "mbele ya uso wako."

SURA YA 11

a Lu 1:67,76

b Mal 3:1
Mt 3:3
Mk 1:2
Lu 1:17
Yoh 3:28c Lu 7:28
Yoh 3:3

d Lu 13:24

e Lu 16:16

f Mal 4:5
Mt 17:10-13

g Lu 7:31-35

h Mt 9:10
Mk 2:15
Yoh 2:2

Safu ya 2

a Lu 5:30
Lu 15:2
Lu 19:7

b Lu 7:34,35

c Yon 3:5,6
Lu 10:13

d Lu 10:14

e Lu 4:31

f Lu 10:15

g Mt 10:15
Lu 10:12h Isa 29:14
Mt 13:15
Lu 10:21
1Ko 1:27

i Yoh 3:35

j Yoh 1:18

nya kodi na watenda dhambi.^a Hata hivyo, hekima huthibitishwa kuwa yenye uadilifu* kupitia kazi zake."^{#b}

20 Kisha Yesu akaanza yakemea majiji ambako alifanya matendo mengi yenye nguvu, kwa sababu hawakutubu: **21** "Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! kwa sababu kama matendo yenye nguvu yaliyofanywa kwenu yangepanywa huko Tiro na Sidoni, watu wa majiji hayo wangepokuwa wametubu zamani katika nguo za magunia na katika majivu.^c **22** Lakini ninawaambia, katika Siku ya Hukumu, itakuwa afadhali zaidi kwa Tiro na Sidoni kuliko kwenu.^d **23** Nawe Kapernaumu,^e je, utainuliwa mpaka mbinguni? Utashuka mpaka Kaburini;^f kwa sababu kama matendo yenye nguvu yaliyofanywa ndani yako yangepanywa huko Sodoma, jiji hilo lingekuwapo mpaka leo hii. **24** Lakini ninawaambia, katika Siku ya Hukumu itakuwa afadhali zaidi kwa nchi ya Sodoma kuliko kwenu."^g

25 Ndipo Yesu akasema: "Ninakusifu hadharani, Baba, Bwana wa mbingu na dunia, kwa sababu umewaficha mambo haya wenye hekima na wenye elimu nawe umeyafunua kwa watoto wadogo.^h **26** Ndiyo, Ee Baba, kwa sababu umekubali iwe hivyo. **27** Baba yangu amenikabidhi vitu vyote,ⁱ na hakuna mtu anayemjua Mwana kika-mili isipokuwa Baba;^j wala hakuna anayemjua Baba kika-mili isipokuwa Mwana, na ye-

11:19 *Au "hutetewa." #Au "kwa matokeo yake." 11:23 *Au "Hadesi." Angalia Kamusi, uku. 2012.

yote ambaye Mwana anapenda kumfunulia.^a **28** Njooi kwangu, nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawaburudisha. **29** Chukueni nira yangu na mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu moyoni,^b nanyi mtapata burudisho kwa ajili yenu.* **30** Kwa maana nira yangu ni laini,* na mzi-go wangu ni mwepesi.”

12 Wakati huo, Yesu alipitia katikati ya mashamba ya nafaka siku ya Sabato. Wanafunzi wake wakahisi njaa wakaanza kukata masuke ya nafaka na kula.^c **2** Mafarisayo walipoona hilo, wamwambia: “Tazama! Wanafunzi wako wanafanya jambo lisilo halali siku ya Sabato.”^d **3** Yesu akawaambia: “Je, hamjasoma alilofanya Daudi wakati yeye na wanaume walio-kuwa pamoja naye walipohisi njaa?”^e **4** Jinsi alivyolingia katika nyumba ya Mungu, nao wakala mikate ya toleo,*^f kitu ambacho hakikuwa halali kwa ke au kwa wale waliokuwa pamoja naye kula, ila makuhani tu?^g **5** Au, je, hamjasoma katika Sheria kwamba siku ya Sabato makuhani huvunja Sabato na wanabaki bila hatia?^h **6** Lakini ninawaambia, hapa pana mtu mkuu kuliko hekalu.ⁱ **7** Hata hivyo, kama mngeelewa maana ya maneno haya, ‘Ninataka rehema/ si dhahihu,’^k hamngewalaumu watu wasio na hatia. **8** Kwa maana Mwana wa binadamu ndiye Bwana wa Sabato.”^l

9 Baada ya kutoka hapo, akaingia ndani ya sinagogi

11:29 *Au “kwa ajili ya nafsi zenu.”
11:30 *Au “rahisi.” 12:4 *Au “mikate iliyowekwa mbele za Mungu.”

SURA YA 11

a Lu 10:22
Yoh 10:15
1Yo 5:20

b Zek 9:9

SURA YA 12

c Kut 12:16
Kum 23:25
Mk 2:23-28
Lu 6:1-5

d Kut 20:10
Kut 31:15
Kum 5:14

e 1Sa 21:1-6

f Kut 25:30
Kut 40:22, 23

g Law 24:5-9

h Hes 28:9
Yoh 7:22

i Lu 11:31, 32

j Mt 23:23

k Ho 6:6
Mik 6:6, 8
Mt 9:13

l Mk 2:27, 28
Lu 6:5

Safu ya 2

a Mk 3:1-6
Lu 6:6-11

b Lu 14:3
Yoh 9:16

c Kut 23:4
Kum 22:4
Lu 14:5

d Mk 3:7

e Mt 8:3, 4
Mk 3:11, 12
Mk 7:35, 36

f Mdo 3:13

g Mt 3:17
Mt 17:5

h Isa 61:1
Mk 1:10

i 2Ti 2:24

j Mt 11:28

k Isa 11:10
Isa 42:1-4
Mdo 4:12

lao, **10** na tazama! kulikuwa na mtu aliyepooza mkono!^a Basi, ili wapate sababu ya kumshtaki wakamuuliza, “Je, ni halali kumponya mtu siku ya Sabato?”^b **11** Akawaambia: “Ukiwa na kondoo mmoja, naye kondoo huyo atumbukie shimoni siku ya Sabato, je, kuna yeyote kati yenu ambaye hatamshika na kumtoa humo?”^c **12** Kwa kweli, mwanadamu ni mwenye thamani sana kuliko kondoo! Basi ni halali kutenda mema siku ya Sabato.” **13** Kisha akamwambia mtu huyo: “Nyoosha mkono wako.” Akaunyoosha, nao ukawa mzima kama ule mkono mwingine. **14** Lakini Mafarisayo wakaenda nje na kupanga njama ili wamuue. **15** Yesu alipojua jambo hilo, akaondoka hapo. Watu wengi wakamfuata,^d naye akawaponya wote, **16** lakini akawaa-giza kwa kusisitiza wasimtangaze,^e **17** ili kutimiza maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii Isaya:

18 “Tazama! Mtumishi wangu^f niliyemchagua, mpendwa wangu, ambaye nimemkubali!^g Nitaweka roho yangu juu yake,^h naye atayatangazia mataifa haki. **19** Hatagombanaⁱ wala kupiga kelele, wala yeyote hatasikia sauti yake kwenye barabara kuu. **20** Hata-ponda tete lililovunjika, wala hatazima utambi unaofifia,^l hadi atakapofanikiwa kuleta haki. **21** Kwa kweli, mataifa yatalitumainia jina lake.”^k

22 Kisha wakamletea mwanamume kipofu aliyekuwa bubu kwa sababu alikuwa na roho mwovu, Yesu

12:18 *Au “nafsi yangu imemkubali.”

akamponya, na yule bubu akaanza kuongea na kuona. **23** Basi, umati wote ukashangaa na kusema: “Je, inawezekana kwamba huyu ndiye Mwana wa Daudi?” **24** Mafarisayo waliposikia jamba hilo wakasema: “Mtu huyu anawafukuza roho waovu kwa nguvu za Beelzebuli,* mtawala wa roho waovu.”^a **25** Akijua fikira zao, akawaambia: “Kila ufalme uliogawanyika dhidi yake wenyewe utaangamia, na kila jiji au nyumba iliogawanyika dhidi yake yenye haitasimama. **26** Vivyo hivyo, ikiwa Shetani anamfukuza Shetani, amegawanyika dhidi yake mwenyewe; basi, ufalme wake utawezaje kusiama? **27** Zaidi ya hayo, ikiwa ninawafukuza roho waovu kupitia Beelzebuli, wana wenu wanawafukuza kupitia nani? Hiyo ndiyo sababu watakuwa waamuzi wenu. **28** Lakini ikiwa ninawafukuza roho waovu kupitia roho ya Mungu, kwa kweli Ufalme wa Mungu umewafikia ninyi ghafla.^b **29** Au yeyote anawezaje kuivamia nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuchukua mali zake isipokuwa kwanza amfungue mtu huyo? Hapo ndipo anaweza kuipora nyumba yake. **30** Yeyote asiye upande wangu ananipinga, na yeyote asiyekusanya pamoja nami anatawanya.^c

31 “Kwa hiyo mimi ninawaambia, watu watasamehewa kila aina ya dhambi na makufuru, lakini yeyote anayekufuru roho takatifu hata samehewa.^d **32** Kwa mfano, yeyote anayesema neno baya

12:24 * Jina lingine la Shetani.

SURA YA 12

a Mk 3:22-27
Lu 11:15-23

b Lu 11:20

c Mk 9:40
Lu 9:50
Lu 11:23

d Mk 3:28, 29
Mdo 7:51
Ebr 6:4, 6

Safu ya 2

a 1Ti 1:13

b Lu 12:10
Ebr 10:26

c Mt 7:17
Lu 6:43

d Mt 3:7
Mt 23:33

e Mt 15:11

f Lu 6:45
Yak 3:6

g Mhu 12:14
Ro 14:12

h Mt 16:1

i Mt 16:4
Lu 11:29-32

j Yon 1:17

dhidi ya Mwana wa binadamu, atasamehewa;^a lakini yeyote anayesema vibaya dhidi ya roho takatifu, hata samehewa, hapana, si katika mfumo huu wa mambo* wala ule utakaokuja.^b

33 “Ufanyeni mti kuwa mzuri na matunda yake yawe mazuri, au muufanye mti uoze na matunda yake yaoze, kwa maana mti hujulikana kwa matunda yake.^c **34** Uzao wa nyoka,^d mnawezaje kusema mambo mema, wakati ninyi ni waovu? Kwa maana kinywa husema mambo yaliyojaa moyoni.^e **35** Mtu mwema hutoa mambo mema katika hazina yake njema, lakini mtu mwovu hutoa mambo mabaya katika hazina yake mbovu.^f **36** Ninawaambia kwamba katika Siku ya Hukumu watu watatoa hesabu^g kuhusu kila neno lisilofaa wanalosema; **37** kwa maneno yako utatangazwa kuwa mwadilifu, na kwa maneno yako utahukumiwa.”

38 Ndipo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu kwa kumwambia: “Mwalimu, tunataka kuona ishara kutoka kwako.”^h **39** Akawajibu: “Kizazi kiovu na chenye uzinzi* kinaendelea kutafuta ishara, lakini hakitapewa ishara yoyote isipokuwa ishara ya nabii Yona.ⁱ **40** Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la samaki mkubwa kwa siku tatu mchana na usiku,^j ndivyo Mwana wa binadamu atakavyokuwa katika moyo wa ardhi siku tatu

12:32 *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mfumo wa mambo.” 12:34 *Au “nyoka-vipiri.” 12:39 *Au “kisicho na uaminifu.”

mchana na usiku.^a **41** Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki nao watakihukumu, kwa sababu walitubu Yona alipowahubiria.^b Lakini tazama! hapa pana mtu mkuu kuliko Yona.^c **42** Malkia wa kusini atasimamishwa katika hukumu pamoja na kizazi hiki naye atakihukumu, kwa sababu alikuja kutoka miisho ya dunia ili asikie hekima ya Sulemani.^d Lakini tazama! hapa pana mtu mkuu kuliko Sulemani.^e

43 "Roho mwovu anapomtoka mtu, yeye hupitia mae-neo yasiyo na maji akitafuta mahali pa kupumzika, lakini hapati.^f **44** Kisha anasema, 'Nitarudi kwenye nyumba yangu niliyohama'; naye anapofika, anakuta haijakaliwa lakini imefagiwa ikawa safi na kupambwa. **45** Naye huenda na kuwaleta roho wengine saba walio waovu kuliko yeye, na baada ya kuingia ndani, wao hukaa humo; na hali ya mwisho ya mtu huyo huwa mbaya zaidi kuliko ya kwanza.^g Hivyo ndivyo itakavyokuwa pia kwa kizazi hiki kiovu."

46 Alipokuwa bado akizungumza na umati, mama yake na ndugu zake^h walikuwa wamesimama nje, wakitaka kuongea naye.ⁱ **47** Basi mtu fulani akamwambia: "Tazama! Mama yako na ndugu zako wamesimama nje, wanataka kuongea nawe." **48** Yesu akamjibu mtu huyo: "Mama yangu ni nani, na ndugu zangu ni nani?" **49** Akinyoosha mkono wake kuelekea wanafunzi wake, akasema: "Tazama! Mama yangu na ndugu zangu!" **50** Kwa maana yeyote anayefanya mapenzi ya Baba yangu

SURA YA 12

a Mt 16:21
Mt 17:23
Mt 27:63
Lu 24:46

b Yon 3:5

c Lu 11:30

d 1Fa 10:1
2Nya 9:1

e Mt 12:6
Lu 11:31

f Lu 11:24-26

g Ebr 6:4, 6
2Pe 2:20

h Mt 13:55
Yoh 2:12
Mdo 1:14
1Ko 9:5
Gal 1:19

i Mk 3:31-35

j Yoh 20:17
Ebr 2:11

Safu ya 2

a Mk 3:35
Lu 8:21

SURA YA 13

b Mk 4:1

c Mt 13:34

d Mk 4:3-9
Lu 8:4-8

e Mt 13:19

f Mt 13:20, 21

g Mt 13:22
Mk 4:18, 19
Lu 8:14

h Mt 13:23
Mk 4:8
Lu 8:8

i Mt 11:15

j Mk 4:10, 11
Lu 8:9, 10

k 1Ko 2:9, 10
Efe 1:9-12
Kol 1:26, 27

l Mt 25:29
Mk 4:25
Lu 8:18

aliye mbinguni, huyo ndiye ndugu yangu, dada yangu, na mama yangu."^a

13 Siku hiyo Yesu akatoka ndani ya nyumba na kuketi kando ya bahari. **2** Na umati mkubwa sana ukakusanyika karibu naye hivi kwamba akapanda ndani ya mashua na kuketi, na umati wote ulikuwa umesimama ufuoni.^b **3** Ndipo akawaambia mambo mengi kwa kutumia mifano,^c akisema: "Tazama! Mpandaji alienda kupanda mbegu.^d **4** Alipokuwa akipanda, mbe-gu fulani zikaanguka kando ya barabara, ndege wakaja na kuzila.^e **5** Nyingine zikaanguka kwenye miamba, mahali pasipo na udongo mwingi, na mara moja zikachipuka kwa sababu udongo haukuwa na kina.^f **6** Lakini jua lilipochomozwa, ziliungua na kunyauka kwa sababu hazikuwa na mizizi. **7** Nyingine zikaanguka kwenye miiba, nayo miiba ikakua na kuzisonga.^g **8** Mbegu nyingine zikaanguka kwenye udongo mzuri nazo zikaanza kuzaa matunda, nyingine mara 100 zaidi, nyingine 60, na nyingine 30.^h **9** Aliye na masikio na asikilize."ⁱ

10 Basi wanafunzi wakaja na kumuuliza: "Kwa nini unazungumza nao kwa kutumia mifano?"^j **11** Akawajibu: "Ninyi mmpewa uwezo wa kuzielewa siri takatifu^k za Ufalme wa mbinguni, lakini wao hawajapewa. **12** Kwa maana yeyote aliye na kitu ataongeze-wa, naye atazidishiwa; lakini yeyote asiye na kitu, hata kile alichu nacho kitachukuliwa.^l **13** Ndiyo maana ninazungumza nao kwa kutumia mifano, kwa sababu, wanatazama

lakini hawaoni, wanasikiliza lakini hawasikii, wala hawaelewi.^a **14** Na unabii wa Isaya unatimia kwao unaosema: 'Kwa kweli mtasikia lakini hamtaelewa, nanyi kwa kweli mtatazama lakini hamtaona.^b **15** Kwa maana mioyo ya watu hawa imekuwa migumu, nao wamesikia kwa masikio yao bila kuitikia, nao wamefungua macho yao, ili wasione kamwe kwa macho yao na kusikia kwa masikio yao na kuelewa kwa masikio yao, kisha waeweke nami niwaponye.^c

16 "Hata hivyo, macho yenu ni yenye furaha kwa sababu yanaona na masikio yenu kwa sababu yanasikia.^d **17** Kwa kweli ninawaambia, manabii wengi na watu waadilifu walitamani kuona mambo mnyayoona lakini hawakuyaoona,^e na kusikia mambo mnyayosikia lakini hawakuyasikia.

18 "Basi, sikilizeni maana ya mfano wa yule mtu aliyeypanda mbegu.^f **19** Mtu yeyote anaposikia neno la Ufalme lakini halielewi, yule mwovu^g huja na kunyakua kilichopandwa moyoni mwake; hiyo ndiyo mbegu iliyopandwa kando ya barabara.^h **20** Na mbegu iliyopandwa kwenye miamba, ni yule anayelisikia neno na kulipokea mara moja kwa shangwe.ⁱ **21** Lakini hana mizizi ndani yake bali anaendelea kwa wakati fulani, hata hivyo dhiki au mateso yakitokea kwa sababu ya lile neno mara moja anakwazika. **22** Na mbegu iliyopandwa kwenye miiba, ni yule anayelisikia neno, lakini mahangaiko ya mfumo huu wa mambo^{*j} na

13:22 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo."

SURA YA 13

a Isa 6:10
Mk 4:12

b Yoh 12:40
Ro 11:8
2Ko 3:14

c Isa 6:9,10
Mk 4:12
Mdo 28:26,27

d Lu 10:23,24

e Yoh 8:56
Efe 3:5
1Pe 1:10

f Mk 4:14
Lu 8:11

g 1Pe 5:8

h Mk 4:15
Lu 8:12

i Mk 4:16,17
Lu 8:13

j Lu 12:22

Safu ya 2

a Mt 6:21
Mk 4:18,19
Mk 10:23
Lu 8:14
1Ti 6:9
2Ti 4:10

b Mk 4:20
Lu 8:15

c Mt 13:38,39

d Ufu 14:15

e Mk 4:30-32
Lu 13:18,19

nguvu za udanganyifu za utajiri hulisonga neno, nalo halizai matunda.^a **23** Na mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri ni wale wanaosikia neno na kulielewa, ambao kwa kweli huzaa matunda, mmoja huzaa mara 100 zaidi, mwingine 60, na mwingine 30."^b

24 Akawatolea mfano mwingine, akisema: "Ufalme wa mbinguni ni kama mtu aliyeypanda mbegu nzuri katika shamba lake. **25** Watu walipokuwa wamelala usingizi, adui yake akaja na kupanda magugu kati ya ngano kisha akaondoka. **26** Ngano ilipoota na kuzaa matunda, magugu pia yalionekana. **27** Kwa hiyo watumwa wa bwana wa nyumba wakaja na kumwambia, 'Bwana, je, hukupanda mbegu nzuri katika shamba lako?' Basi magugu yametoka wapi?' **28** Aka-waambia, 'Adui, mtu fulani, ndiye aliyefanya hivyo.'^c Watumwa wakamuuliza, 'Basi, je, unataka twende tukayang'oe?' **29** Akasema, 'Hapana, ili mnapong'oa magugu, msije mkang'oa ngano pia. **30** Acheni vikue pamoja mpaka wakati wa mavuno, na katika majira ya mavuno nita-waambia wavunaji: Kusanyeni magugu kwanza na kuyafunga matita-matita ili yateketewe motoni; kisha mkusanye ngano ghalani mwangu."^d

31 Akawatolea mfano mwingine akisema: "Ufalme wa mbinguni ni kama mbegu ya haradali ambayo mtu aliichukua na kuipanda katika shamba lake.^e **32** Kwa kweli, mbegu hiyo ni ndogo kuliko mbegu zote, lakini inapokua huwa kubwa kuliko mi-

mea yote ya mboga na huwa mti, hivi kwamba ndege wa angani huja na kupata makao katika matawi yake.”

33 Akawaambia mfano mwingine: “Ufalme wa mbinguni ni kama chachu* ambayo mwanamke aliichukua na kuchanganya na vipimo vikubwa vitatu vya unga, mpaka unga wote ukachacha.”^a

34 Yesu alizungumza mambo hayo yote na umati kwa kutumia mifano. Kwa kweli, hakuwa akizungumza nao bila mfano,^b **35** ili kutimiza maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii: “Nitafungua kinywa changu kwa mifano; nitatanga mambo yaliyofichwa tangu kuwekwa msingi.”^c

36 Baada ya kuuaga umati, akaingia ndani ya nyumba. Wanafunzi wake wakajaja na kumwambia: “Tufafanulie ule mfano wa magugu katika shamba.” **37** Akawajibu: “Mpandaji aliyepanda mbegu nzuri ni Mwana wa binadamu; **38** lile shamba ni ulimwengu.^d Nazo mbegu nzuri ni wana wa Ufalme, lakini magugu ni wana wa yule mwovu,^e **39** na adui aliyepanda magugu ni Ibilisi. Mavuno ni umalizio wa mfumo wa mambo,* na wavunaji ni malaika. **40** Kwa hiyo, kama vile magugu hukusanywa na kuteketezwa kwa moto, ndivyo itakavyokuwa katika umalizio wa mfumo wa mambo.^f **41** Mwana wa binadamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika Ufalme wake vitu vyote vinavyosababisha kukwazi-

13:33 *Au “hamira.” #Au “ukaumuka.”
13:35 *Au labda, “kuumbwa kwa ulimwengu.” 13:39, 40, 49 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 13

a Lu 13:21

b Mk 4:33, 34

c Zb 78:2

d Mt 24:14
Ro 10:18
Kol 1:6

e Yoh 8:44

f Mt 13:30

Safu ya 2

a Mt 13:30

b Amu 5:31

c Flp 3:7

d Flp 3:8

e Law 11:9

f Law 11:12

ka na watu wenye mazoea ya kuasi sheria, **42** nao watawatupa ndani ya tanuru la moto.^a Humo ndimo watalia na kusaga meno yao. **43** Wakati huo waadilifu watang'aa kwa uangavu kama jua^b katika Ufalme wa Baba yao. Aliye na masikio na asikilize.

44 “Ufalme wa mbinguni ni kama hazina iliyofichwa katika shamba, ambayo mtu fulani aliipata na kuificha; na kwa sababu ya shangwe aliyo nayo, anaenda na kuuza kila kitu alichu nacho na kununua shamba hilo.^c

45 “Tena Ufalme wa mbinguni ni kama mfanyabiashara anayesafiri akitafuta lulu nzuri. **46** Alipopata lulu moja yenye thamani kubwa, alienda na mara moja akauza vitu vyote alivyokuwa navyo na kuinunua.^d

47 “Tena Ufalme wa mbinguni ni kama wavu wa kukotwa ulioshushwa baharini, ukavua samaki wa kila aina. **48** Ulipojaa waliuvuta hadi ufuoni, nao wakaketi na kuwaweka samaki wazuri^e ndani ya vyombo, lakini wakawatupa wale wasiofaa.^f **49** Hivyo ndivyo itakavyokuwa katika umalizio wa mfumo wa mambo.* Malaika wataenda kuwatenganisha waovu kutoa kwa waadilifu. **50** Nao watawatupa waovu ndani ya tanuru la moto. Humo ndimo watalia na kusaga meno yao.

51 “Je, mmelewa mambo hayo yote?” Wakamjibu: “Ndiyo.” **52** Ndipo akawaambia: “Ikiwa ni hivyo, kila mwalimu wa watu wote, anapofundishwa kuhusu Ufalme wa mbinguni ni kama bwana wa nyumba, ambaye hutoa katika

hazina yake vitu vipya na pia vya zamani.”

53 Yesu alipomaliza kutoa mifano hiyo akaondoka hapo. **54** Baada ya kuingia katika eneo lake la nyumbani,^a akaanza kuwafundisha katika sinagogi lao, hivi kwamba wakashangaa na kuuliza: “Mtu huyu alipata wapi hekima hii na matendo haya yenye nguvu?”^b **55** Je, huyu si mwana wa yule seremala?^c Je, mama yake haitwi Maria, na ndugu zake Yakobo, Yosefu, Simoni, na Yuda?^d **56** Na dada zake, je, wote hawako pamoja nasi? Basi, alipata wapi mambo haya yote?”^e **57** Kwa hiyo, wakaanza kukwazika kwa sababu yake.^f Lakini Yesu akawaambia: “Nabii anaheshimiwa kila mahali isipokuwa katika eneo lake la nyumbani na katika nyumba yake mwenyewe.”^g **58** Naye hakufanya matendo mengi yenye nguvu huko kwa sababu hawakuwa na imani.

14 Wakati huo Herode, mtawala wa wilaya,^{*} akasikia habari kumhusu Yesu.^h **2** Akawaambia watumishi wake: “Huyu ni Yohana Mbatizaji. Alifufuliwa kutoka kwa wafu na ndiyo sababu anafanya matendo yenye nguvu.”ⁱ **3** Herode^{*} alikuwa amemkamata Yohana akamfunga na kumtia gerezeni kwa sababu ya Herodia, mke wa Filipo ndugu yake.^j **4** Kwa maana Yohana alikuwa aki-mwambia: “Si halali kwako kuwa na mwanamke huyo.”^k **5** Hata hivyo, ingawa Herode alitaka kumuua, aliugopa umati, kwa sababu wali-

14:1 *Tnn., “tetraki.” 14:3 *Yaani, Herode Antipa. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 13

a Mt 2:23

b Mk 6:1-6

c Lu 4:22
Yoh 6:42d Mt 12:46
Yoh 2:12
Mdo 1:14
1Ko 9:5
Gal 1:19

e Yoh 7:15

f 1Pe 2:7, 8

g Mk 6:4
Lu 4:24
Yoh 4:44

SURA YA 14

h Mk 6:14
Lu 9:7-9
Mdo 4:27i Mt 16:13, 14
Mk 6:16j Mk 6:17, 18
Lu 3:19, 20k Law 18:16
Law 20:21

Safu ya 2

a Mk 6:20
Lu 1:67, 76

b Mwa 40:20-22

c Mk 6:21-29

d Mk 6:25

e Mk 6:31-33
Lu 9:10f Mt 9:36
Mt 15:32
Mk 1:41
Mk 6:34
Lu 7:13
Ebr 2:17
Ebr 5:2

g Lu 9:11

h Mk 6:35-44
Lu 9:12-17
Yoh 6:5-13

mwona kuwa nabii.^a **6** Lakini wakati wa sherehe ya siku-kuu ya kuzaliwa kwa Herode,^b binti ya Herodia alicheza dansi na kumfurahisha sana Herode^c **7** hivi kwamba akaahidi kwa kiapo kumpa chochote ambacho angeomba. **8** Ndiyo yule binti, akichochea na mama yake, akasema: “Nipe kwenye sinia kichwa cha Yohana Mbatizaji.”^d **9** Mfalme akahuzunika, lakini kwa sababu ya viapo alivyotoa mbele ya wageni^{*} wake, akaamuru apewe kichwa hicho. **10** Basi akawatuma watu gerezeni, nao wakamkata Yohana kichwa. **11** Kichwa chake kikaletwa kwenye sinia akapewa yule msichana, naye akampelekea mama yake. **12** Baadaye wanafunzi wake wakaja wakaondoa maiti hiyo na kuizika, kisha wakaenda kumjulisha Yesu. **13** Yesu aliposikia hilo, akaondoka hapo kwa mashua, akaenda mahali pasipo na watu ili awe peke yake. Lakini umati ulipopata habari, ukamfuata kwa miguu kutoka katika majiji.^e

14 Alipofika ufuoni, akaona umati mkubwa, akawasikiti-^f kua na kuwaponya wagonjwa wao.^g **15** Lakini ilipofika jioni, wanafunzi wake wakaja na kumwambia: “Mahali hapa hapana watu na muda umesonga sana; uambie umati uondoke, waende vijijini wakinunulie chakula.”^h **16** Hata hivyo, Yesu akawaambia: “Si lazima waondoke; ninyi wapeni chakula.” **17** Wakamwambia: “Hatuna kitu hapa isipokuwa mikate mitano na sama-

14:9 *Au “wale waliokuwa wameketi mezani.”

ki wawili tu.” **18** Akasema: “Nileteeni hapa.” **19** Akauagiza umati uketi kwenye nyasi. Kisha akachukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akatoa baraka^a na baada ya kumi-mega mikate, akawapa wanafunzi, nao wanafunzi wakau-gawia umati. **20** Basi wote wakala wakashiba, nao wakakusanya vipande vilivyobaki, wakajaza vikapu 12.^b **21** Sasa wale waliokula walikuwa wanaume karibu 5,000, na pia wanawake na watoto wadogo.^c **22** Kisha, bila kukawia, akawaagiza wanafunzi wake wapande mashua na kumtangu-lia kwenda ng’ambo ya bahari, huku yeye akiuaga umati.^d

23 Baada ya kuuaga umati, akapanda mlimani akiwa peke yake ili kusali.^e Ilipofika jioni, alikuwa peke yake huko. **24** Kufikia sasa mashua ilikuwa mamia ya mita* kuto-ka kwenye nchi kavu, ikitaa-bishwa na mawimbi kwa sababu upepo ulikuwa ukivuma kinyume chao. **25** Lakini katika kesho la nne la usiku* akawajia, akitembea juu ya bahari. **26** Wanafunzi walipomwona akitembea juu ya bahari, wakahangaika na kusema: “Ni mzuka!” Wakapaza sauti kwa hofu. **27** Lakini mara moja Yesu akawaambia: “Jipeni moyo! Ni mimi; msiogope.”^f **28** Petro akamjibu: “Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako nikitembea juu ya maji.” **29** Akamwambia: “Njoo!” Ndipo Petro akatoka kwenye ma-

14:24 *Tnn., “stadia nyingi.” Stadiumo moja ilikuwa sawa na mita 185 (futi 606.95). **14:25** *Yaani, karibu saa 9 usiku hadi saa 12 asubuhi.

SURA YA 14

a Mt 15:36
Mk 6:41
Lu 9:16

b 2Fa 4:42-44
Mk 6:42, 43
Mk 8:8
Lu 9:17
Yoh 6:12, 13

c Mk 6:44
Lu 9:14
Yoh 6:10

d Mk 6:45-52
Yoh 6:16-21

e Mk 6:46
Lu 6:12
Lu 9:18

f Mk 6:50
Yoh 6:20

Safu ya 2

a Mt 6:30
Mt 8:26
Mt 28:16, 17
Yak 1:6

b Mk 6:53-56

c Mt 9:20, 21
Mk 3:10
Lu 6:19

SURA YA 15

d Mt 7:1, 2

e Lu 11:38
Yoh 2:6

f Mt 15:9
Mk 7:8-13
Kol 2:8

g Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:2

h Kut 21:17
Law 20:9

shua, akatembea juu ya maji kumwelekea Yesu. **30** Lakini alipoitazama ile dhoruba ya upepo akaogopa. Alipoanza kuzama, akapaza sauti: “Bwana, niokoe!” **31** Mara moja Yesu akaunyoosha mko-no wake, akamshika na kumwambia: “Wewe mwenye imani ndogo, kwa nini ume-kuwa na shaka?”^a **32** Walipopanda kwenye mashua, ile dhoruba ikatulua. **33** Ndipo wale waliokuwa ndani ya mashua wakamsujudia* wakise-ma: “Kwa kweli wewe ni Mwana wa Mungu.” **34** Basi wakavuka na kufika kwenye nchi kavu huko Genesareti.^b

35 Watu wa huko walipomtambua, wakaeneza habari katika maeneo yote yali-yokuwa karibu, basi watu wakamletea wagonjwa wote. **36** Nao wakamsihi awaruhusu waguse tu upindo wa vazi lake la nje,^c na wote waliou-gusa wakaponywa kabisa.

15 Ndipo Mafarisayo na waandishi kutoka Yerusalemu wakamjia Yesu^d waki-sema: **2** “Kwa nini wanafunzi wako huvunja mapokeo ya mababu zetu? Kwa mfano, hawanawi* mikono kabla ya kula.”^e

3 Akawajibu: “Kwa nini ninyi pia huvunja amri ya Mungu kwa sababu ya mapokeo yenu?”^f **4** Kwa mfano, Mungu alisema, ‘Mheshimu baba yako na mama yako,’^g na, ‘Yeyote anayemtukana* baba yake au mama yake anapaswa kuuawa.’^h **5** Lakini ninyi mnasema, ‘Yeyote anayemwambia baba yake au mama

14:33 *Au “wakamwinamia.” **15:2** *Yaani, hawajisafishi kishererehe. **15:4** *Au “anayesema mambo mabaya kuhusu.”

yake: “Chochote nilicho nacho ambacho kingekusaidia ni zawadi iliyowekwa wakfu kwa Mungu.”^a **6** hahitaji kamwe kumheshimu baba yake.’ Kwa hiyo, mmelibatilisha neno la Mungu kwa sababu ya mapokeo yenu.^b **7** Ninyi wanafiki, kwa kufaa Isaya alitabiri kuwahuu aliposema:^c **8** ‘Watu hawa huniheshimu kwa midomo yao, lakini moyo yao iko mbali nami. **9** Wao huniabu-bu bure, kwa maana wanafundisha amri za wanadamu kuwa mafundisho.”^d **10** Ndipo akaita umati ukaribie na kuwaambia: “Sikilizeni na kuelewa maneno haya:”^e **11** Mtu hachafuliwi na kile kinacholingia kinywani mwake, bali huchafuliwa na kile kinachotoka kinywani mwake.”^f

12 Ndipo wanafunzi wakaja na kumwambia: “Unajua kwa mba Mafarisayo walikwazika waliposikia mambo uliyosema?”^g **13** Akawajibu: “Kila mmea ambao Baba yangu wa mbinguni hakuupanda utang’olewa. **14** Waacheni. Wao ni viongozi vipofu. Basi, kipofu akimwongoza kipofu, wote wawili watatumbukia ndani ya shimo.”^h **15** Petro akamwambia: “Tufafanulie mfanano huo.” **16** Ndipo akasema: “Je, ninyi pia bado hamwelewi?”ⁱ **17** Je, hamjui kwamba chochote kinacholingia kinywani hupita tumboni kisha hutoka na kuingia chooni? **18** Hata hivyo, mambo yanayotoka kinywani hutoka moyoni, nayo ndiyo yanayomchafua mtu.^j **19** Kwa mfano, moyoni hutoka mawazo mabaya: k mauaji, uzinzi, uasherati,*

15:19 *Wingi wa neno la Kigiriki *porne’a*. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 15

a Mk 7:11, 12

b Mk 7:13

c Mk 7:6

d Isa 29:13
Mk 7:7

e Mk 7:14

f Mk 7:15
Efe 4:29
Yak 3:6

g Mk 7:17

h Mt 23:15, 16
Lu 6:39

i Mk 7:18-23

j Mk 7:20

k Mwa 8:21
Yer 17:9

Safu ya 2

a Mk 7:24

b Mk 7:25-30

c Isa 53:6
Mt 10:5, 6
Mdo 3:26
Mdo 13:46
Ro 15:8

d Mk 7:28

e Mk 7:31

wizi, ushahidi wa uwongo, na makufuru. **20** Hayo ndiyo mambo yanayomchafua mtu; lakini kula bila kunawa* miko-no hakumchafui mtu.”

21 Yesu akatoka hapo na kwenda katika eneo la Tiro na Sidoni.^a **22** Na tazama! mwanamke fulani Mfoinike kutoka eneo hilo akamjia, akapaza sauti: “Nihurumie,* Bwana, Mwana wa Daudi. Binti yangu anasumbuliwa kikati-li na roho mwovu.”^b **23** Lakini Yesu hakumjibu mwanamke huyo. Kwa hiyo wanafunzi wake wakaja na kumwambia: “Mwambie aende, kwa sababu anaendelea kutufuata akipaza sauti.” **24** Yesu akajibu: “Sikutumwa kwa yeyote isipokuwa kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.”^c **25** Lakini mwanamke huyo akaja na kumsujudia* akisema: “Bwana, nisaidie!” **26** Yesu akamjibu: “Haifai kuuchukua mkate wa watoto na kuwatupia mbwa wadogo.” **27** Mwanamke huyo akasema: “Ndiyo Bwana, lakini hata hao mbwa wadogo hula makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza ya mabwana wao.”^d **28** Ndipo Yesu akamwambia: “Ewe mwanamke, imani yako ni kubwa; na itendeke kama unavyotaka.” Na kuanzia saa hiyo binti yake akapona.

29 Yesu akaondoka hapo na kwenda karibu na Bahari ya Galilaya,^e kisha akapanda mlimani, akaketi huko. **30** Ndipo umati mkubwa ukamjia, na kuwaleta watu waliokuwa viwete, vilema, vipofu, mabubu,

15:20 *Yaani, bila kujisafisha kisherehe.

15:22 *Au “Nionyeshe rehema.”

15:25 *Au “kumwinamia.”

na wengine wengi, nao waka-waweka miguuni pake, naye akawaponya.^a **31** Basi umati ukashangaa ulipoona mabubu wakiongea, vilema wakiponywa, viwete wakitembea, na vipofu wakiona, nao wakamsifu Mungu wa Israeli.^b

32 Lakini Yesu akawaita wanafunzi wake na kuwambia: “Ninausikitikia umati,^c kwa sababu tayari wamekaa pamoja nami siku tatu nao hawajala chochote. Sitaki kuwaacha waende wakawa na njaa,* wasije wakazi-mia njiani.”^d **33** Hata hivyo, wanafunzi wakamwambia: “Tutapata wapi mikate ya kutosha kuushibisha umati huu mkubwa mahali hapa pasipo na watu?”^e **34** Ndipo Yesu akawauliza: “Mna mikate mingapi?” Wakajibu: “Saba, na samaki wachache wadogo.” **35** Kwa hiyo, baada ya kuuagiza umati uketi chini, **36** akachukua ile mikate saba na wale samaki, na baada ya kutoa shukrani, akamega na kuanza kuwagawia wanafunzi, nao wanafunzi wakaugawia umati.^f **37** Na wote wakala wakashiba, kisha wakakusanya vipande vilivyobaki, wakajaza vikapu saba vikubwa.^g **38** Sasa wale waliokula walikuwa wanaume 4,000, na pia wanawake na watoto wadogo. **39** Mwishowe, baada ya kuuaga umati, akaingia kwenye mashua na kwenda katika eneo la Magadani.^h

16 Mafarisayo na Masadukayo wakamjia Yesu, na ili kumjaribu wakamwomba awaonyeshe ishara kutoka mbinguni.ⁱ **2** Akawajibu:

15:32 *Au “wamefunga.”

SURA YA 15

a Isa 35:5
Mt 19:2
Mk 3:10

b Mt 9:33

c Mt 14:14
Mk 6:34

d Mk 8:1-9

e 2Fa 4:42-44

f Mt 14:19

g Mk 8:8, 9

h Mk 8:10

SURA YA 16

i Mt 12:38
Mk 8:11
Lu 11:16

Safu ya 2

a Mk 8:12

b Yon 1:17
Mt 12:39
Lu 11:29

c Mk 8:13-21

d Mk 8:15
Lu 12:1

e Mt 14:17

f Mt 15:34

g Lu 12:1

“Inapofika jioni ninyi husema, ‘Hali ya hewa itakuwa nzuri kwa maana anga ni jekundu,’ **3** na asubuhi mnasema: ‘Leo kutakuwa na baridi kali na mvua, kwa maana anga ni jekundu na lina mawingu mazito.’ Mnajua jinsi ya kufafanua hali ya anga, lakini hamwezi kufafanua ishara za nyakati. **4** Kizazi kiovu na chenye uzinzi* kinaendelea kutafuta ishara, lakini hakitapewa ishara yoyote^a isipokuwa ishara ya Yona.”^b Ndipo akawaacha, akaenda zake.

5 Sasa wanafunzi wakavuka kwenda ng'ambo ya bahari lakini wakasahau kuchukua mikate.^c **6** Yesu akawambia: “Muwe macho na mjihadhari na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.”^d **7** Basi wakanza kujadiliana, wakisema: “Hatukubeba mikate yoyote.” **8** Akijua hilo, Yesu akawauliza: “Ninyi wenye imani ndogo, kwa nini mnajadiliana kati yenu kuhusu kutokuwa na mikate? **9** Je, bado hamwelewi, au je, hamkumbuki ile mikate mitano kuhusiana na wale watu 5,000, na ni vikapu vingapi mlivyokusanya?^e **10** Au ile mikate saba kuhusiana na wale watu 4,000 na ni vikapu vingapi vikubwa mlivyokusanya?^f **11** Kwa nini hamwelewi kwamba sikuongea nanyi kuhusu mikate? Bali jihadharini na chachu* ya Mafarisayo na Masadukayo.”^g **12** Ndipo wakaelewa kwamba hakuwa akizungumza kuhusu chachu ya mikate, bali kujihadhari na mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo.

16:4 *Au “kisicho na uaminifu.” 16:11 *Au “hamira.”

13 Alipofika katika eneo la Kaisaria Filipi, Yesu akawauliza wanafunzi wake: “Watu wanasema Mwana wa binadamu ni nani?”^a **14** Wakajibu: “Baadhi yao husema Yohana Mbatizaji,^b wengine Eliya,^c na bado wengine Yere-mia au mmoja wa manabii.”

15 Akawauliza: “Hata hivyo, ninyi mnasema mimi ni nani?” **16** Simoni Petro akajibu: “Wewe ndiye Kristo,^d Mwana wa Mungu aliye hai.”^e

17 Yesu akamwambia: “Mwenye furaha ni wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa sababu mwili ni damu havikukufunulia* hilo, bali Baba yangu aliye mbinguni ndiye aliyekufunulia.^f **18** Pia, nina-kuambia: Wewe ni Petro,^g na juu ya mwamba^h huu nitajenga kutaniko langu, na malango ya Kaburi* hayatalishinda. **19** Nitakupa funguo za Ufalme wa mbinguni, na lolote utakalofunga duniani tayari litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalofungua duniani tayari litakuwa limefunguliwa mbinguni.” **20** Ndipo akawaagiza wanafunzi kwa kuisitiza wasimwambie yeyote kwamba yeye ndiye Kristo.ⁱ

21 Tangu wakati huo, Yesu akaanza kuwafanulia wanafunzi wake kwamba ni lazima aende Yerusalemu na kuteswa sana na wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi, kisha atauawa, na siku ya tatu afufuliwe.^j **22** Ndipo Petro akampeleka kando na kuanza kumkemea, akisema: “Bwana

16:17 *Au “kwa sababu mwanadamu hakukufunulia.” 16:18 *Au “Hadesi.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 16

a Mk 8:27-29

Lu 9:18-20

b Mt 14:1, 2

c Yoh 1:25, 26

d Mk 8:29

Lu 9:20

Yoh 1:40, 41

Yoh 4:25

Yoh 11:27

e Zb 2:7

Mt 14:33

Mdo 9:20, 22

Ebr 1:2

1Yo 4:15

f Mt 11:27

g Yoh 1:42

h Ro 9:33

1Ko 3:11

1Ko 10:4

Efe 2:20

1Pe 2:6-8

i Mk 8:29, 30

Lu 9:20, 21

j Zb 16:10

Isa 53:12

Mt 17:22, 23

Mt 20:18, 19

Mk 8:31

Lu 9:22

Lu 24:46

1Ko 15:3, 4

Safu ya 2

a Mk 8:32

b Mk 8:33

c Mt 10:38

Mk 8:34

Lu 9:23

Lu 14:27

d Mk 8:35

Lu 9:24

Lu 17:33

Yoh 12:25

Ufu 12:11

e Mk 8:36

Lu 9:25

f Zb 49:8

g Zb 62:12

Met 24:12

Lu 9:26

Ro 2:6

1Pe 1:17

h Mt 17:2

Mk 9:1

Lu 9:27

SURA YA 17

i Mk 9:2-8

Lu 9:28-36

j Ufu 1:13, 16

jihurumie;* hutapatwa kamwe na mambo hayo.”^a **23** Lakinini Yesu akamgeuzia mgongo, akamwambia Petro: “Nenda nyuma yangu, Shetani! Wewe ni kikwazo kwangu, kwa sababu hufikirii mawazo ya Mungu, bali ya wanadamu.”^b

24 Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake: “Mtu yeyote akitaka kunifuata, lazima ajikane mwenyewe, aubebe mti wake wa mateso* na aendelee kunifuata.^c **25** Kwa maana yeyote anayetaka kuuokoa uhai wake* ataupoteza, lakini yeyote anayeupoteza uhai wake* kwa ajili yangu ataupata.^d **26** Kwa kweli mtu atapata faida gani akiupata ulimwengu wote lakini apoteze uhai wake? *^e Au mtu atatoa nini ili abadilishane na uhai wake? *^f

27 Kwa maana Mwana wa binadamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake, kisha atamlipa kila mtu kulingana na mwendo wake.^g **28** Kwa kweli ninawaambia kwamba kuna baadhi ya wale waliosimama hapo ambao hawataonja kifo kamwe kabla ya kumwona Mwana wa binadamu akija katika Ufalme wake.”^h

17 Siku sita baadaye, Yesu alienda pamoja na Petro, Yakobo na Yohana ndugu yake kwenye mlima mrefu wakiwa peke yao.ⁱ **2** Msuru yake ikageuka mbele yao; uso wake ukang’aa kama jua, na mavazi yake ya nje yakang’aa* kama nuru.^j **3** Tazama! wakaona Musa na Eliya wakizunguma

16:22 *Au “jitendee kwa fadhili.” 16:24 *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mti wa mateso.” 16:25, 26 *Au “nafsi yake.” 17:2 *Au “yakawa meupe.”

na Yesu. **4** Ndipo Petro akamwambia Yesu: “Bwana, ni vizuri sisi tuwe hapa. Ukitaka, nitasimamisha mahema matatu hapa, moja lako, moja la Musa, na moja la Eliya.” **5** Alipokuwa bado akizungumza, tazama! wingu jangavu likawafunika, na tazama! sauti kutoka katika lile wingu ikasema: “Huyu ni Mwanangu, mpendwa, ambaye nimemkubali.”^a Msikilizeni.”^b **6** Wanafunzi waliposikia hilo wakaaunguka kifudifudi, wakaogopa sana. **7** Ndipo Yesu akawakaribia, akawagusa na kuwaambia: “Simameni. Msiogope.” **8** Walipotazama juu, hawakumwona mtu yeyote ila Yesu tu. **9** Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani, Yesu akawaamuru: “Msimwambie mtu yeyote maono hayo mpaka Mwana wa binadamu atakapofuiliwa kutoka kwa wafu.”^c

10 Hata hivyo, wanafunzi wakamuuliza: “Kwa nini basi waandishi husema kwamba lazima Eliya aje kwanza?”^d **11** Akawajibu: “Kwa kweli Eliya anakuja naye atarudisha mambo yote.”^e **12** Hata hivyo, ninawaambia kwamba tayari Eliya amekuja lakini hawakumtambua bali walimtendea kama walivyotaka.^f Vivyo hivyo, Mwana wa binadamu atateseka mikononi mwao.”^g **13** Ndipo wanafunzi wakatambua kwamba alikuwa akiwaeleza kumhusu Yohana Mbatizaji.

14 Walipofika karibu na umati,^h mtu fulani akamkaribia Yesu, akapiga magoti, na kusema: **15** “Bwana, mhurumie* mwanangu, kwa saba-

17:15 *Au “mwonyeshe rehema.”

SURA YA 17

a Zb 2:7
Isa 42:1
Mt 3:17
2Pe 1:17, 18

b Kum 18:15
Mk 9:7
Lu 9:35
Mdo 3:22, 23
Ebr 2:3

c Mt 16:20
Mk 9:9

d Mk 9:11

e Isa 40:3
Mal 4:5, 6
Mt 11:13, 14
Mk 9:12
Lu 1:17

f Mk 9:13

g Mt 16:21
Lu 23:24, 25

h Lu 9:37

Safu ya 2

a Mk 9:17-29
Lu 9:38-42

b Kum 32:5, 20

c Mt 8:13
Mt 9:22
Mt 15:28
Yoh 4:51, 52

d Mt 21:21
Mk 11:23
Lu 17:6

e Mt 20:18
Lu 9:44, 45

f Mt 16:21
Mk 9:31

g Kut 30:13, 14

bu ana kifafa na ni mgonjwa sana. Yeye huanguka ndani ya moto na ndani ya maji mara nyingi.^a **16** Nili-mleta kwa wanafunzi wako, lakini walishindwa kumpoonya.” **17** Yesu akajibu: “Enyi kizazi kisicho na imani na kili-chopotoka,^b nitaendelea kuwa pamoja nanyi mpaka lini? Nitawavumilia mpaka lini? Mleteni hapa.” **18** Kisha Yesu akamkemea yule roho mwovu, naye akamtoka, na yule mvulana akapona kuanzia saa hiyo.^c **19** Ndipo wanafunzi wakamjia Yesu faraghani na kumuuliza: “Kwa nini tulishindwa kumfukuza?” **20** Aka-waambia: “Ni kwa sababu ya imani yenu ndogo. Kwa kweli ninawaambia, mkiwa na imani inayolingana na mbegu ya haradali, mtauambia mlima huu, ‘Ondoka hapa uende pale,’ nao utaondoka, na hakuna jambo litakalowashinda.”^d **21** *—

22 Walipokuwa wamekusanyika huko Galilaya, Yesu akawaambia: “Mwana wa binadamu atasalitiwa mikononi mwa watu,^e **23** nao wata-muua, na siku ya tatu atafuiliwa.”^f Kwa hiyo wakahuzunika sana.

24 Baada ya kufika Kapernaumu watu wanaokusanya kodi ya drakma* mbili wakaja na kumuuliza Petro: “Je, mwalimu wenu hulipa kodi ya drakma mbili?”^g **25** Akajibu: “Ndiyo.” Hata hivyo, mara tu alipoingia ndani ya nyumba Yesu akamuuliza: “Unaona-je Simoni? Wafalme wa dunia hupokea ushuru au kodi*^h

17:21 *Angalia Nyongeza A3. 17:24 *Angalia Nyongeza B14. 17:25 *Au “kodi ya kichwa.”

kutoka kwa nani? Kutoka kwa wana wao au kutoka kwa wageni?" **26** Alipojibu: "Kutoka kwa wageni," Yesu akamwambia: "Basi, kwa kweli wana hawalipi kodi. **27** Lakini ili tusiwakwaze,^a nenda baharini utupe ndoano na uchukue samaki wa kwanza atakayetokea, na utakapofungua kinywa chake, utapata sarafu ya fedha.* Ichukue nawe uwa-
pe kwa ajili yangu na kwa ajili yako."

18 Katika saa hiyo wanafunzi wakamkaribia Yesu na kumuuliza: "Kwa kweli ni nani aliyekuwa zaidi katika Ufalme wa mbinguni?"^b **2** Basi akamwita mtoto mdogo, akamsimamisha katikati yao **3** na kusema: "Kwa kweli ninawaambia, msipogeuka* na kuwa kama watoto wadogo,^c hamtaingia kamwe katika Ufalme wa mbinguni."^d **4** Kwa hiyo, yeyote atakayejinyenyekeza kama mtoto huyu mdogo ndiye mkuu zaidi katika Ufalme wa mbinguni;^e **5** na yeyote anayempokea mtoto mdogo kama huyu kwa msingi wa jina langu ananipokea mimi pia. **6** Lakini yeyote anayemkwaza mmoja wa hawa wadogo wanaoniamini, ingekuwa afadhali afungiwe shingoni jiwe la kusagia ambalo huzungushwa na punda, kisha azamishwe baharini.^f

7 "Ole kwa ulimwengu kwa sababu ya vikwazo! Bila shaka, lazima vikwazo vije, lakini ole wake mtu ambaye ki-kwazo kitakuja kupitia kwake!

17:27 *Tnn., "sarafu ya stateri," inadhaniwa kuwa ndiyo tetradrakma. Angalia Nyongeza B14. 18:3 *Au "msipobadilika."

SURA YA 17

a 1Ko 10:32
2Ko 6:3

SURA YA 18

b Mk 9:33-37
Lu 9:46-48
Lu 22:24

c Mt 19:14
Ipe 2:2

d Lu 18:17

e Mt 15:33
Mt 20:26
Mt 23:12
Lu 9:48
Lu 14:11
Lu 22:26
Yak 4:10
Ipe 5:5

f Mk 9:42
Lu 17:1, 2

Safu ya 2

a Kol 3:5

b Mt 25:41
Mk 9:43-48

c Mt 5:22
Mt 5:29
Mk 9:47
Ro 8:13

d Lu 1:19
Ebr 1:7, 14

e Ipe 2:25

f Lu 15:3-7

g 2Pe 3:9

h Law 19:17
Met 25:8, 9
Lu 17:3

i Yak 5:20

j Kum 19:15
2Ko 13:1
1Ti 5:19

8 Basi, ikiwa mkono wako au mguu wako unakufanya ukwazike, ukate na kuutupa mbali nawe.^a Ni afadhali uingie katika uzima ukiwa kilema au kiwete kuliko kutupwa ndani ya moto wa milele ukiwa na mikono miwili au miguu miwili.^b **9** Pia, ikiwa jicho lako linakufanya ukwazike, ling'oe na kulitupa mbali nawe. Afadhali uingie katika uzima ukiwa na jicho moja kuliko kutupwa katika Gehena* ya moto ukiwa na macho mawili.^c **10** Angalieni msimdharau mmoja wa hawa wadogo, kwa maana ninawaambia kwamba malaika zao mbinguni sikuzote huutazama uso wa Baba yangu aliyekuwa mbinguni.^d **11** *—

12 "Mnaonaje? Mtu akiwa na kondoo 100 na mmoja apotee,^e je, hatawaacha wale 99 mlimani na kwenda kumtafuta yule aliyepotea?^f **13** Naye akimpata, hakika ninawaambia, yeye humshangilia huyo kuliko wale 99 ambao hawakupotea. **14** Vivyo hivyo, Baba yangu* aliyekuwa mbinguni hape-
ndi hata mmoja wa hawa wadogo aangamie.^g

15 "Zaidi ya hayo, ndugu yako akitenda dhambi, nenda ufunue kosa lake* kati yako na yeye peke yenu.^h Akikusikiliza, umempata ndugu yako.ⁱ **16** Lakini asipokusikiliza, nenda pamoja na mtu mmoja au wawili, ili kwa ushahidi wa* mashahidi wawili au watatu kila jambo lithibitishwe.^j **17** Asipowasikiliza hao, liambie kutaniko. Asipolisikili-

18:9 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 18:11 *Angalia Nyongeza A3. 18:14 *Au labda, "yenu." 18:15 *Tnn., "na umkaripie." 18:16 *Tnn., "kinywa cha."

za kutaniko pia, na awe kwa-ko kama mtu wa mataifa^a na kama mkusanya kodi.^b

18 “Kwa kweli ninawaambia, mambo yoyote mtakayofunga duniani tayari yatakuwa yamefungwa mbinguni, na mambo yoyote mtakayofunga duniani tayari yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.

19 Tena kwa kweli ninawaambia, wawili kati yenu duniani wakikubaliana kuomba jambo lolote muhimu, litatendeka kwa ajili yao kwa sababu ya Baba yangu aliye mbinguni.^c

20 Kwa maana mahali wanapokusanyika wawili au watatu katika jina langu,^d nipo hapo kati yao.”

21 Ndipo Petro akaja na kumuuliza: “Bwana, ndugu yangu atanitendea dhambi mara ngapi nami nimsamehe? Mpaka mara saba?” **22** Yesu akamwambia: “Ninakuambia, si mpaka mara saba, bali mpaka mara 77.^e

23 “Ndiyo sababu Ufalme wa mbinguni ni kama mfalme aliyetaka kufanya hesabu pamoja na watumwa wake.

24 Alipoanza kufanya hesabu, akaletewa mtu aliyekuwa na deni lake la talanta 10,000.*

25 Lakini kwa sababu hakuwa na uwezo wa kulipa, bwana wake akaamuru wamuuze mtumwa huyo, mke wake, watoto wake, na mali zake zote ili kulipa deni.^f **26** Ndipo mtumwa huyo akaanguka chini na kumsujudia,* akisema, ‘Naomba univumilie, nitakulipa kila kitu.’ **27** Bwana wake akamsikitikia mtu-

18:24 *Talanta 10,000 za fedha zilikuwa sawa na dinari 60,000,000. Angalia Nyongeza B14. **18:26** *Au “kumwianamia.”

SURA YA 18

a Yoh 18:28
Mdo 10:28
Mdo 11:2, 3

b Ro 16:17
1Ko 5:11

c Mk 11:24
Yoh 14:13
Yoh 16:23, 24
1Yo 3:22
1Yo 5:14

d 1Ko 5:4, 5

e Mt 6:12
Mk 11:25
Lu 17:4
Efe 4:32
Kol 3:13

f Kut 21:7
Law 25:39
2Fa 4:1
Ne 5:8

Safu ya 2

a 1Yo 1:9

b Isa 55:7
Mt 6:12
Mt 7:12
Yak 2:13

c Ro 2:6

d Mt 6:14
Mk 11:25
Lu 17:3
Efe 4:32

SURA YA 19

e Mk 10:1

f Kum 24:1
Mk 10:2-12

mwa huyo, akamwachilia na kulifuta deni lake.^a **28** Lakini mtumwa huyo alipotoka akamkuta mmoja wa watumwa wenzake aliyekuwa na deni lake la dinari* 100, akamshika na kumkaba koo, akisema, ‘Nilipe ninachokudai.’

29 Basi mtumwa mwenzake akaanguka chini na kuanza kumsihi, ‘Naomba univumilie, nami nitakulipa.’ **30** Hata hivyo, akakataa, akaenda na kuagiza atupwe gerezani mpaka alipe deni lake. **31** Watumwa wenzake walipoona jambo hilo, wakahuzunika sana, wakaenda kumweleza bwana wao mambo yote yaliyokuwa yametendeka. **32** Ndipo bwana wake akamwita na kumwambia: ‘Mtumwa mwovu, nilifuta deni lako lote uliponisihii. **33** Je, hukupaswa pia kumwonyesha rehema mtumwa mwenzako kama nilivyokuonyesha rehema?’^b

34 Ndipo bwana wake akiwa amekasirika sana, akamkabi-dhi kwa walinzi wa jela mpaka alipe deni lake lote. **35** Baba yangu wa mbinguni atawatendea ninyi vivyo hivyo^c ikiwa kila mmoja wenu hatamsamehe ndugu yake kutoka moyoni.”^d

19 Yesu alipomaliza kusema maneno hayo, akaondoka Galilaya na kwenda kwenye mipaka ya* Yudea ng’ambo ya Yordani.^e **2** Pia, umati mkubwa ukamfuata, naye akawaponya huko.

3 Mafarisayo wakaja wakisudia kumjaribu Yesu, wamuuliza: “Je, ni halali mwanamume kumtaliki mke wake kwa sababu yoyote ile?”^f

18:28 *Angalia Nyongeza B14. **19:1** *Au “karibu na mipaka ya.”

4 Akawajibu: “Je, hamkusoma kwamba yule aliyewaumba tangu mwanzo aliwaumba mwanamume na mwanamke^a

5 na kusema: ‘Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye atashikamana na mke wake, na hao wawili watakuwa mwili mmoja?’^b **6** Basi wao si wawili tena, bali mwili mmoja. Kwa hiyo, kile ambacho Mungu ameunganisha mtu yeyote asikitenganishe.”^c **7** Wakamuuliza: “Basi, kwa nini Musa aliagiza kutoa cheti cha kumfukuza na kumtaliki?”^d

8 Akawajibu: “Musa aliwaruhusu kuwataliki wake zenu kwa sababu ya ugumu wa miyo yenu,^e lakini haikuwa hivyo tangu mwanzo.^f **9** Ninawaambia kwamba mtu yeyote anayemtaliki mke wake isipokuwa kwa sababu ya uasherati,^{*} na kumwoa mwingine, anafanya uzinzi.”^g

10 Wanafunzi wakamwambia: “Ikiwa hali iko hivyo kati ya mtu na mke wake, ni afadhali mtu asioe.” **11** Yesu akawaambia: “Si watu wote wanaolipa nafasi jambo hilo, ila tu wale walio na zawadi.”^h

12 Kwa maana kuna wale waliozaliwa wakiwa matowashi, wengine wamefanywa matowashi na watu, na wengine wamejifanya wenyewe kuwa matowashi kwa ajili ya Ufalme wa mbinguni. Yule anayeweza kulipa nafasi jambo hilo na afanye hivyo.”ⁱ

13 Ndipo watu wakamletea watoto wadogo ili aweke mikono yake juu yao na kusali, lakini wanafunzi wakawakemea.^j **14** Hata hivyo,

19:9 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 19

a Mwa 1:27

Mwa 5:2

b Mwa 2:24

Efe 5:31

c Mk 10:9

1Ko 7:11

d Kum 24:1

Mt 5:31

e Mk 10:5

f Mwa 2:24

g Mal 2:14

Mt 5:32

Mk 10:11, 12

Lu 16:18

Ro 7:3

1Ko 7:10

Ebr 13:4

h 1Ko 7:7

i 1Ko 7:32, 38

1Ko 9:5

j Mk 10:13-16

Lu 18:15-17

Safu ya 2

a Mt 18:3

Mk 10:14

Lu 18:16

b Mk 10:17-22

Lu 18:18-23

c Mk 10:18

d Law 18:5

Lu 10:25-28

e Kut 20:13

Kum 5:17

f Kut 20:14

Kum 5:18

g Kut 20:15

Kum 5:19

h Kut 20:16

Kum 5:20

i Kut 20:12

Kum 5:16

j Law 19:18

Mt 22:39

Mk 12:31

Lu 10:27

Ro 13:9

k Mt 6:20

l Lu 12:33

Lu 18:22

Flp 3:7

m Lu 18:23

n Mk 10:23

Lu 18:24

1Ti 6:10

Yesu akawaambia: “Waacheni watoto wadogo waje kwangu, na msijaribu kuwazuia, kwa maana Ufalme wa mbinguni ni wa wale walio kama wao.”^a **15** Naye akaweka mikono yake juu yao kisha akaondoka hapo.

16 Sasa tazama! mtu fulani akamjia na kumuuliza: “Mwalimu, ninapaswa kufanya mambo gani mema ili nipate uzima wa milele?”^b **17** Yesu akamwambia: “Kwa nini unaniuliza kuhusu mambo mema? Kuna Mmoja tu aliye mwe-ma.^c Hata hivyo, ikiwa unataka kuingia katika uzima, zishi-ke amri sikuzote.”^d **18** Akamuuliza: “Amri gani?” Yesu akajibu: “Usiue,^e usifanye uzinzi,^f usiibe,^g usitoe ushahidi wa uwongo,^h **19** mheshimu baba yako na mama yako,ⁱ na lazima umpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.”^j **20** Yule mwanamume kijana akamwambia: “Nimeyashika yote hayo; nifanye nini zaidi?” **21** Yesu akamwambia: “Ikiwa unataka kuwa mkamilifu,^{*} nenda ukauze mali zako na uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni;^k kisha uje uwe mfuasi wangu.”^l **22** Yule mwanamume kijana aliposikia hivyo, akaenda zake akiwa na huzuni, kwa maana alikuwa na mali nyingi.^m **23** Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake: “Kwa kweli nina-waambia, itakuwa vigumu kwa tajiri kuingia katika Ufalme wa mbinguni.ⁿ **24** Tena ninawaambia, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri

19:21 *Au “kamili.”

kuingia katika Ufalme wa Mungu.”^a

25 Wanafunzi waliposikia hilo, wakashangaa sana na kumuuliza: “Ni nani kwa kweli anayeweza kuokolewa?”^b **26** Yesu akawatazama kwa makini na kusema: “Kwa wanadamu jambo hilo haliwezekani, lakini kwa Mungu mambo yote yanawezekana.”^c

27 Ndipo Petro akamwambia: “Tazama! Tumeacha kila kitu na kukufuata; basi tutapata nini?”^d **28** Yesu akasema: “Kwa kweli ninawaambia, katika uumbaji mpya, Mwana wa binadamu atakapoketi katika kiti chake cha ufalme chenye utukufu, ninyi ambao mmenifuata mtaketi katika viti vya ufalme 12, mkiyahukumu makabila 12 ya Israeli.”^e **29** Na kila mtu ambaye ameaacha nyumba au ndugu au dada au baba au mama au watoto au mashamba kwa ajili ya jina langu atapokea mara 100 zaidi, naye ataurithi uzima wa milele.^f

30 “Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na wa mwisho watakuwa wa kwanza.”^g

20 “Kwa maana Ufalme wa mbinguni ni kama bwana mwenye nyumba aliyetoka asubuhi na mapema kwenenda kuajiri wafanyakazi kwa ajili ya shamba lake la mizabibu.”^h **2** Baada ya kukubaliana na wafanyakazi hao awalipe dinari* moja kwa siku, akawatuma katika shamba lake la mizabibu. **3** Akatoka pia karibu saa tatu,* akaona wengine wamesimama sokoni bila

20:2, 9, 10, 13 *Angalia Nyongeza B14.
20:3 *Yaani, karibu saa 3 asubuhi.

SURA YA 19

a Mk 10:25
Lu 18:25

b Mk 10:26, 27
Lu 18:26, 27

c Ayu 42:2

d Mk 10:28
Lu 5:11
Lu 18:28
Flp 3:8

e Da 7:14
Mt 20:21
Lu 22:28-30
1Ko 6:2
Ufu 20:4

f Mk 10:29, 30
Lu 18:29, 30
Ebr 10:34

g Mt 20:16
Mk 10:31
Lu 13:30

SURA YA 20

h Mt 21:33

Safu ya 2

a Law 19:13
Kum 24:14, 15

b Mt 20:2

kazi; **4** akawaambia, ‘Ninyi pia, nendeni katika shamba la mizabibu, nami nitawalipa haki yenu.’ **5** Basi wakaenda. Tena akatoka karibu saa sita* na saa tisa* na kufanya vivyo hivyo. **6** Mwishowe, akatoka karibu saa kumi na moja,* akakuta wengine wakiwa wamesimama tu, naye akawauliza, ‘Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi?’ **7** Wakamjibu, ‘Kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri.’ Akawaambia, ‘Ninyi pia nendeni katika shamba la mizabibu.’

8 “Ilipofika jioni, mwenye shamba la mizabibu akamwambia msimamizi wake, ‘Waite wafanyakazi uwalipe mshahara wao,’^a ukianza na wa mwisho na kumalizia na wa kwanza.’ **9** Wale watu wa saa 11 walipokuja, wakupokea kila mmoja dinari* moja. **10** Basi, wale wa kwanza walipokuja, walidhani wangepokea zaidi; lakini wao pia wakalipwa dinari* moja. **11** Walipoipokea wakaanza kumlalamikia bwana mwenye nyumba **12** na kusema, ‘Watu hawa wa mwisho walifanya kazi kwa saa moja tu; na bado umewalipa sawa na sisi tuliofanya kazi ngumu mchana kutwa kwenye jua kali!’ **13** Lakini akamjibu mmoja wao, akasema, ‘Mwenzangu, sijakukosea. Tulikubaliana dinari* moja, si vyo?’^b **14** Chukua mshahara wako uende. Ninataka kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe. **15** Je, sina haki ya kufanya kile ninachotaka na vitu vyangu? Au jicho lako lina

20:5 *Yaani, karibu saa 6 mchana.
*Yaani, karibu saa 9 alasiri. 20:6
*Yaani, karibu saa 11 jioni.

lako lina wivu* kwa sababu mimi ni mwema?"^a **16** Vivyo hivyo, wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho."^b

17 Alipokuwa akipanda kwenda Yerusalem, Yesu akawaita Faragani wale wanafunzi 12 na kuwaambia wakiwa barabarani:^c **18** "Tazama! Tunapanda kwenda Yerusalem, na Mwana wa binadamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi. Nao watamhukumia kifo"^d **19** na kumtia mikononi mwa watu wa mataifa ili wamdhaki, wampige mijeledi, na kumuua kwenye mti;^e na siku ya tatu atafuuliwa."^f

20 Ndipo mama ya wana wa Zebedayo^g akamjia akiwa na wanawe, akamsujudia* na kumwomba jambo fulani.^h **21** Yesu akamuuliza: "Unataka nini?" Akamjibu: "Toa agizo kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja upande wako wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto, katika Ufalme wako."ⁱ **22** Yesu akajibu: "Hamjui kile mnachoomba. Je, mnaweza kunywa kikombe ambacho niko karibu kukinywa?"^j Wakamwambia: "Tunaweza." **23** Akawaambia: "Kwa kweli mtakunywa kikombe changu,^k lakini kukeiti upande wangu wa kuume na upande wangu wa kushoto si haki yangu kutoa, bali wataketi wale ambao Baba yangu amewatayarishia."^l

24 Wale wengine kumi waliposikia jambo hilo, waka-wakasirikia hao ndugu wawi-

20:15 *Tnn., "ni baya; lina uovu." ^aAu "mkarimu." 20:20 *Au, "akamw-namia."

SURA YA 20

a Mt 6:23

b Mt 19:30
Mk 10:31
Lu 13:30c Mk 10:32
Lu 18:31d Mt 16:21
Mk 10:33, 34
Lu 9:22
Lu 18:32, 33e Mt 27:31
Yoh 19:1f Mt 17:22, 23
Mt 28:6
Mdo 10:40
1Ko 15:4g Mt 4:21
Mt 27:55, 56

h Mk 10:35-40

i Mt 19:28

j Mt 26:39
Mk 10:38
Mk 14:36
Yoh 18:11k Mdo 12:2
Ro 8:17
2Ko 1:7
Ufu 1:9

l Mk 10:39, 40

Safu ya 2

a Mk 10:41-45
Lu 22:24

b Mk 10:42

c 2Ko 1:24
1Pe 5:3d Mt 18:4
Mt 23:11
Mk 10:43, 44
Lu 22:26

e Mk 9:35

f Lu 22:27
Yoh 13:14
Flp 2:7g Isa 53:11
Mk 10:45
1Ti 2:5, 6
Tit 2:13, 14
Ebr 9:28h Mt 9:27
Mk 10:46-52
Lu 18:35-43

i Mt 9:29

SURA YA 21

j Mk 11:1-3
Lu 19:28-31

li.^a **25** Lakini Yesu akawaita, akawaambia: "Mnajua kwamba watawala wa mataifa hupiga ubwana juu yao na wakuu hutumia mamlaka juu yao."^b **26** Haipaswi kuwa hivyo kati yenu;^c bali yeyote anayetaka kuwa mkubwa kati yenu lazima awe mhudumu wenu,^d **27** na yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kati yenu lazima awe mtumwa wenu.^e **28** Kama vile Mwana wa binadamu alivyokuja, si kuhudumiwa, bali kuhudumu^f na kutoa uhai wake* uwe fidia badala ya wengi."^g

29 Walipokuwa wakitoka Yeriko umati mkubwa ukamfuata. **30** Na tazama! wanaume wawili vipofu walio-kuwa wameketi kando ya barabara waliposikia kwamba Yesu anapitia hapo, wakapaza sauti: "Bwana, Mwana wa Daudi, tuhurumie!"^h

31 Hata hivyo, umati ukawa-kemea na kuwaambia wanyamaze; lakini wakapaza sauti hata zaidi, wakisema: "Bwana, Mwana wa Daudi, tuhurumie!"* **32** Basi Yesu akasimama, akawaita na kuwauliza: "Mnataka niwafanyie nini?" **33** Wakamjibu: "Bwana, tunaomba macho yetu yafunguliwe." **34** Yesu akawa-sikitikia, akayagusa macho yao,ⁱ na mara moja wakaanza kuona, nao wakamfuata.

21 Walipokaribia Yerusalem kwenye Mlima wa Mizeituni, Yesu akawatama wanafunzi wawili,^j 2 akawaambia: "Nendeni katika kijiji mtakachokiona, na mara moja mta-

20:28 *Au "nafsi yake." 20:30, 31 *Au "tuonyeshe rehema!"

mwona punda amefungwa, na mwanapunda akiwa pamoja naye. Wafungueni na kuniletea. **3** Mtu yeyote akiwauliza, semeni, 'Bwana anawahitaji.' Na mara moja atawaruhusu mwachukue."

4 Kwa kweli hilo lilitukia ili kutimiza maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii: **5** "Mwambieni binti ya Sayuni, 'Tazama! Mfalme wako anakuja kwako,'^a naye ni mpole^b na amepanda juu ya punda, naam, juu ya mwanapunda, uzao wa mnyama wa kubeba mizigo."^c

6 Kwa hiyo wale wanafunzi wakaenda na kufanya kama Yesu alivyowaagiza.^d **7** Wakamleta huyo punda na mwanapunda wake, kisha wakatandika juu yao mavazi yao ya nje, naye akayakalia.^e **8** Wengi katika umati wakataandaza mavazi yao ya nje barabarani,^f na wengine wakatata matawi ya miti na kuyatandaza barabarani. **9** Isitoshе umati uliomtangulia na wale waliomfuata waliendelea kupaza sauti: "Tunaomba umwokoe, Mwana wa Daudi!^g Amebarikiwa yule anayekuja katika jina la Yehova!^h Tunaomba umwokoe, katika vilele vilivyvo juu!"ⁱ

10 Alipokuwa Yerusalemu, jiji lote likawa na msukosuko, na kuulizana: "Ni nani huyu?"

11 Umati ukaendelea kusema: "Huyu ndiye nabii Yesu,^j kutoka Nazareti ya Galilaya!"

12 Yesu akaingia hekaluni na kuwafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadili

SURA YA 21

a Isa 62:11
Yoh 12:15

b Mt 11:29

c Zek 9:9

d Mk 11:4-6
Lu 19:32-35

e 1Fa 1:38, 40
Mk 11:7-11
Yoh 12:14, 15

f Lu 19:36-38

g Mt 9:27
Mt 21:15

h Zb 118:25, 26
Yoh 12:13

i Mk 11:9, 10

j Mt 21:46
Lu 7:16
Lu 24:19

Safu ya 2

a Mk 11:15, 16
Lu 19:45
Yoh 2:15

b Isa 56:7

c Yer 7:11
Mk 11:17
Lu 19:46
Yoh 2:16

d Mt 21:9

e Mk 11:18
Lu 19:39, 40

f Zb 8:2

g Mk 11:11
Lu 21:37
Yoh 11:1

h Mk 11:12

i Lu 13:6

j Mt 3:10
Mk 11:13, 14

k Mk 11:20, 21

l Mt 17:20
Mk 11:22, 23
Lu 17:6

m Mk 11:24
Lu 11:9
Yoh 14:13
Yak 1:5
1Yo 3:22

pesa na viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa.^a **13** Aka waambia: "Imeandikwa, 'Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala,'^b lakini ninyi mnaifanya kuwa pango la wanyang'anyi."^c **14** Pia, vipofu na vilema wakamwendea hekaluni, naye akawaponya.

15 Wakuu wa makuhani na waandishi walipoona mambo ya kustaajibisha aliyofanya na pia wavulana waliokuwa wakipaza sauti hekaluni wakisema: "Tunaomba umwokoe, Mwana wa Daudi!"^d waka kasirika^e **16** na kumwambia: "Je, unasikia wanachosema?" Yesu akajibu: "Ndiyo. Je, hamkusoma jambo hili, 'Kutoka katika vinywa vya watoto wadogo na wanaonyonya, ume toa sifa?'"^f **17** Kisha akawaacha, akatoka nje ya jiji na kwenda Bethania, akalala huko.^g

18 Alipokuwa akirudi jijini asubuhi na mapema, akahisi njaa.^h **19** Akaona mtini kando ya barabara, akaukaribia lakini hakupata chochote ila majani tu,ⁱ akauambia: "Usizae matunda tena kamwe."^j Mara moja ule mtini ukanyauka. **20** Wanafunzi walipoona hilo, wakashangaa na kusema: "Kwa nini mtini huu umenyauka mara moja?"^k **21** Yesu akawajibu: "Kwa kweli nina waambia, mkiwa na imani nanyi msiwe na shaka, hamtafanya tu nilichoufanyia mtini huo, bali hata mkiuambia mlima huu, 'Ng'oka, ukatupwe baharini,' jambo hilo litatendeka."^l **22** Na mambo yote mnayoomba katika sala, mkiwa na imani, mtapokea."^m

23 Baada ya kuingia hekaluni, wakuu wa makuhani na wazee wa watu wakaja

alipokuwa akifundisha, waka-muuliza: “Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Na ni nani aliyekupa mamlaka hayo?”^a **24** Yesu akawajibu: “Nami nitawauliza swali. Mkinijibu basi nitawaambia ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani: **25** Ubatizo wa Yohana, ulitoka wapi? Ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?”^{*} Lakini wakaanza kujadiliana kati yao wakisema: “Tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’ atatuuliza, ‘Kwa nini hamkumwamini?’^b **26** Lakini tukisema, ‘Ulitoka kwa wanadamu,’ tunaogopa umati, kwa maana wote wanamwona Yohana kuwa nabii.” **27** Basi wakamjibu: “Hatujui.” Naye Yesu akawaambia: “Nami siwaambii ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani.

28 “Mnaonaje? Mtu fulani alikuwa na watoto wawili. Akamwendea wa kwanza, akamwambia, ‘Mwanangu, leo nenda ukafanye kazi katika shamba la mizabibu.’ **29** Akamjibu, ‘Sitaenda,’ lakini baadaye akajuta na akaenda. **30** Akamwendea wa pili na kumwambia jambo hilihilo. Naye akamjibu, ‘Nitaenda Baba,’ lakini hakwenda. **31** Kati ya hao wawili ni yupi aliyefanya mapenzi ya baba yake?” Wakasema: “Yule wa kwanza.” Yesu akasema: “Kwa kweli ninawaambia wakusanya kodi na makahaba wanawatangulia ninyi kuingia katika Ufalme wa Mungu. **32** Kwa maana Yohana alikuja kwenu katika njia ya uadilifu, lakini hamkumwamini. Hata hivyo, wakusanya kodi

21:25 *Au “chanzo chake ni wanadamu?”

SURA YA 21

a Mk 11:27-33
Lu 20:1-8

b Mt 21:32
Mk 11:30, 31
Lu 7:29, 30

Safu ya 2

a Lu 3:12
Lu 7:29, 30

b Isa 5:7

c Isa 5:2

d Mk 12:1-9
Lu 20:9-16

e Ne 9:26

f 2Nya 36:15
Mdo 7:52
Ebr 11:32, 37

g Ebr 1:2

h Mdo 2:23
Mdo 3:15

na makahaba walimwamini,^a nanyi, ijapokuwa mliiona hilo, hamkujuta na kumwamini.

33 “Sikilizeni mfano mwingine: Kulikuwa na mtu aliyemiliki shamba, akapanda shamba la mizabibu^b na kulizungushia ua, akachimba shinikizo la divai* ndani yake, akajenga mnara;^c kisha akalikodisha kwa wakulima, naye akasafiri kwenenda ng’ambo.^d **34** Majira ya matunda yalipofika, akawatuma watumwa wake kwa wakulima ili wakachukue matunda yake. **35** Hata hivyo, wakulima hao wakawakamata wale watumwa, mmoja wakampiga, mwingine wakamuua, na mwingine wakampiga mawe.^e **36** Akawatuma tena watumwa wengine, wengi zaidi ya wale wa kwanza, lakini wakawatendea vivyo hivyo.^f **37** Mwishowe akamtuma mwana wake kwao, akisema, ‘Watamheshimu mwanangu.’ **38** Wakulima walipomwona yule mwana wakaambiana, ‘Huyu ndiye mrithi.^g Njooi tumuue ili tuuchukue urithi wake!’ **39** Kwa hiyo wakamkamata, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu na kumuua.^h **40** Basi, mwenye shamba la mizabibu atakapokuja, atawatendea nini wakulima hao?” **41** Wakamwambia: “Kwa sababu ni waovu, atawaangamiza kabisa na kulikodisha shamba la mizabibu kwa wakulima wengine, ambao watampa matunda yatakapoiva.”

42 Yesu akawaambia: “Je, hamkusoma kamwe katika Maandiko kwamba ‘Jiwe

21:33 *Au “mahali pa kukamulia zabibu.”

ambalo wajenzi walilikataa limekuwa jiwe kuu la pembeni.*^a Hili limetoka kwa Yehova,[#] na ni lenye kustaajibisha machoni petu?'^b **43** Ndiyo sababu ninawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kweni na kupewa taifa linalozaa matunda yake. **44** Pia, mtu atakayeanguka kwenye jiwe hilo atavunjika vipandevipande.^c Na litamponda yeyote litakayemwangukia."^d

45 Wakuu wa makuhani na Mafarisayo waliposikia mifano ya Yesu, wakajua kwamba alikuwa akizungumza kuwahuu.^e **46** Ingawa walitaka kumkamata, waliogopa umati, kwa sababu walimwona kuwa nabii.^f

22 Yesu akasema tena nao akitumia mifano, aka-waambia: **2** "Ufalme wa mbinguni ni kama mfalme aliye-mwandalia mwanawe karamu ya ndoa.^g **3** Akawatuma watumwa wake wawaite wale walioalikwa kwenye karamu ya ndoa, lakini hawakutaka kuja.^h **4** Tena akawatuma watumwa wengine, akasema, 'Waambieni wale walioalikwa: "Tazameni! Nimetayarisha chakula changu cha mchana, ng'ombe dume wangu na wanyama waliononeshwa wamechinjwa, na vitu vyote viko tayari. Njooi kwenye karamu ya ndoa."ⁱ **5** Lakini wakupuuza na kwenda zao, wengine kwenye mashamba yao, na wengine kwenye biashara zao;ⁱ **6** lakini wengine wakawakamata wale watumwa wakawatendea kwa dhara-rau na kuwaua.

21:42 *Tnn., "kichwa cha pembeni."
#Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 21

a Isa 28:16
Lu 20:17
Mdo 4:11
Ro 9:33
Efe 2:20
1Pe 2:7

b Zb 118:22, 23
Mk 12:10, 11

c Isa 8:14
1Pe 2:7, 8

d Lu 20:18

e Mk 12:12
Lu 20:19

f Mt 21:11
Yoh 7:40

SURA YA 22

g Lu 14:16
Ufu 19:9

h Lu 14:17, 18

i Lu 14:18, 19

Safu ya 2

a Da 9:26

b Mdo 13:45, 46

c Mt 21:43
Lu 14:23

d Mk 12:13-17
Lu 20:20-26

e Mk 3:6

7 "Mfalme akakasirika sana, akatuma majeshi yake yakawau wauaji hao na kulichoma jiji lao.^a **8** Kisha akawaambia watumwa wake, 'Karamu ya ndoa iko tayari, lakini walioalikwa hawakustahili.^b **9** Kwa hiyo, nendeni kwenye barabara zinazotoka jijini, na kumwalika kwenye karamu ya ndoa mtu yeyote mtakayemwona.'^c **10** Basi watumwa wakaenda barabarani na kuwaalika wote waliowaona, waovu na wema; na chumba cha sherehe za harusi kikajaa wageni.*

11 "Mfalme alipoingia kuwakagua wageni, akamwona mtu ambaye hakuwa amevaa vazi la ndoa. **12** Basi akamuuliza, 'Mwenzangu, umeingiaje humu bila vazi la ndoa?' Akakosa la kusema. **13** Ndipo mfalme akawaambia watumishi wake, 'Mfungeni mikono na miguu, kisha mmtupe nje gizani. Huko ndiko atalia na kusaga meno yake.'

14 "Kwa maana kuna wengi walioalikwa, lakini waliochaguliwa ni wachache."

15 Ndipo Mafarisayo wakaenda kupanga njama pamoja ili wamtege Yesu kwa maneno yake.^d **16** Basi wakawatuma wanafunzi wao kwake, pamoja na wafuasi wa chama cha Herode.^e Wakamwambia: "Mwalimu, tunajua wewe husema ukweli nawe hufundisha njia ya Mungu katika kweli, na hutafuti kibali cha yeyote, kwa maana huangalii sura ya nje ya mtu. **17** Basi tuambia, unaonaje? Je, ni halali*

22:10 *Au "wale waliokuwa wameketi mezani." 22:17 *Au "sawa."

au si halali kumlipa Kaisari kodi?"* **18** Lakini Yesu aki-jua uovu wao, akasema: "Kwa nini mnanijaribu, ninyi wanafiki? **19** Nionyesheeni sarafu ya kodi." Wakamletea dinari.*

20 Akawauliza: "Sura hii na maandishi haya ni ya nani?"

21 Wakajibu: "Ni ya Kaisari." Ndipo akawaambia: "Basi, mlipeni Kaisari vitu vya Kaisari, na Mungu vitu vya Mungu."^a

22 Waliposikia hilo, wakashangaa, wakamwacha na kwenenda zao.

23 Siku hiyo, Masadukayo ambao husema hakuna ufufuo,^b wakaja na kumuuliza:^c

24 "Mwalimu, Musa alisema: 'Mtu yeyote akifa bila kupata watoto, ndugu yake anapaswa kumwoa mke wake ili kumwinulia ndugu yake uzao.'^d

25 Basi kulikuwa na ndugu saba kati yetu. Wa kwanza akaoa kisha akafa, na kwa sababu hakuwa na watoto, akamwachia ndugu yake mke wake. **26** Ikawa vivyo hivyo kwa yule wa pili na wa tatu, na kwa wote saba. **27** Mwishowe, yule mwanamke akafa. **28** Basi, katika ufufuo, atakuwa mke wa nani kati ya wale saba? Kwa maana aliolewa na wote."

29 Yesu akawajibu: "Ninyi mmekosea, kwa sababu hamjui Maandiko wala nguvu za Mungu;^e **30** kwa maana katika ufufuo, wanaume hawaoi, wala wanawake hawaoilewi, bali wao ni kama malaika mbinguni.^f **31** Kuhusu ufufuo wa wafu, je, hamkusoma mliiloambiwa na Mungu, aliposema: **32** 'Mimi ni Mungu wa

22:17 *Au "kodi ya kichwa." 22:19 *Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 22

a Da 3:17, 18
Mal 3:8
Mk 12:17
Lu 20:25
Lu 23:2
Ro 13:7

b Mdo 4:1, 2
Mdo 23:8

c Mk 12:18-23
Lu 20:27-33

d Mwa 38:7, 8
Kum 25:5, 6
Ru 1:11
Ru 3:13

e Mk 12:24-27

f Lu 20:35, 36

Safu ya 2

a Kut 3:6

b Lu 20:37, 38
Ro 4:17

c Mt 7:28
Mk 11:18

d Mk 12:28

e Kum 6:5
Kum 10:12
Yos 22:5
Mk 12:30
Lu 10:27

f Law 19:18
Mk 12:31
Lu 10:27
Kol 3:14
Yak 2:8
1Pe 1:22

g Ro 13:10
Gal 5:14

h Mk 12:35-37
Lu 20:41-44

i Yoh 7:42

j 2Sa 23:2

k Zb 110:1
Mdo 2:34, 35
1Ko 15:25
Ebr 1:13
Ebr 10:12, 13

l Mk 12:37

Abrahamu na Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo?'"^a Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai."^b **33** Umati uliposikia hilo, ukashangazwa na mafundisho yake.^c

34 Mafarisayo waliposikia kwamba Yesu amewanyamazi-sha Masadukayo, wakaja wakiwa kikundi kimoja. **35** Na mmoja wao aliyekuwa na ujuzi wa Sheria, akamuuliza swali ili kumjaribu: **36** "Mwalimu, ni amri gani iliyo kuu zaidi katika Sheria?"^d **37** Akamwambia: "Lazima umpende Yehova* Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi[#] yako yote na kwa akili yako yote."^e

38 Hii ndiyo amri ya kwanza na iliyo kuu zaidi. **39** Ya pili, kama hiyo, ni hii, 'Lazima umpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.'^f

40 Sheria yote na Manabii hutegemea amri hizo mbili."^g

41 Basi Mafarisayo walipo-kuwa wamekusanyika, Yesu akawauliza:^h **42** "Mna maoni gani kuhusu Kristo? Ni mwana wa nani?" Wakamwambia: "Wa Daudi."ⁱ **43** Akawauliza: "Basi, kwa nini Daudi akiongozwa na roho^j anamwita Bwana, akisema, **44** 'Yehova* alimwambia Bwana wangu: 'Keti kwenye mkono wangu wa kuume mpaka ni waweke maadui wako chini ya miguu yako'?"^k **45** Basi ikiwa Daudi anamwita Bwana, anawezaje kuwa mwanawe?"^l **46** Na hakuna mtu aliyeweza kumjibu neno, na tangu siku hiyo hakuna mtu aliyethubutu tena kumuuliza swali.

22:37, 44 *Angalia Nyongeza A5. 22:37 [#]Angalia Kamusi, uku. 2012.

23 Ndipo Yesu akauambia umati pamoja na wanafunzi wake: **2** “Waandishi na Mafarisayo wamejiketisha kwenye kiti cha Musa. **3** Kwa hiyo, fanyeni mambo yote wanayowaambia, lakini msitende kama wao, kwa maana wao husema lakini hawatendi mambo wanayosema.^a **4** Wao hufunga mizigo mizito na kuiweka kwenye mabega ya watu,^b lakini wao weneye hawataki kuisogeza hata kwa kidole chao.^c **5** Kazi zote wanazofanya, wanazifanya ili waonwe na watu,^d kwa maana wanapanua visanduku vyenye maandiko wanavyovaa kama ulinzi,^{*e} na kurefusha pindo zenye nyuzi za mavazi yao.^f **6** Wao hupenda mahali penye heshima zaidi kwenye milo ya jioni na viti vya mbele^{*} katika masinagogi^g **7** na kusalimiwa sokoni na kuitwa Rabi^{*} na watu. **8** Lakini ninyi, msiitwe Rabi, kwa maana Mwalimu^h wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. **9** Zaidi ya hayo, msimwite mtu yeyote baba yenu duniani, kwa maana Baba yenu ni mmoja, Yule aliye mbinguni. **10** Wala msiitwe viongozi, kwa maana Kiongozi wenu ni mmoja, Kristo. **11** Lakini aliye mkuu zaidi kati yenu lazima awe mhudumu wenu.ⁱ **12** Yeyote anayejiinua atanyenyekezwa,^k na yeyote anajinyenyekeza atainuliwa.^l **13** “Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! kwa sababu mnawafungia watu Ufalme wa mbinguni; kwa maana ninyi wenyewe hamwingii, na

23:5 *Au “wanapanua vibweta vyao.”
23:6 *Au “bora.” 23:7 *Au “Mwalimu.”

SURA YA 23

a Mal 2:7, 8

b Mt 11:28

c Lu 11:46

d Mt 6:1, 2

e Kum 6:6, 8

f Hes 15:38, 39

g Mk 12:38, 39
Lu 11:43
Lu 14:7, 10
Lu 20:46

h Yoh 13:13

i Mt 6:9

j Mt 20:26
Mk 9:35
Lu 22:26

k Met 16:18

l Mt 29:23
Mt 18:4
Lu 14:11
Ro 12:3
1Pe 5:5

Safu ya 2

a Lu 11:52

b Mt 6:2
Lu 12:56

c Mt 15:14

d Mt 5:34, 35

e 1Fa 8:13

f Law 27:30

g Mik 6:8
Yoh 7:24h Mt 9:13
Mt 12:7

mnawazuia wale wanaotaka kuingia.^a **14** *—

15 “Ole wenu, waandishi na Mafarisayo wanafiki!^b kwa sababu mnasafiri baharini na kwenye nchi kavu ili kumgeuzi imani mtu mmoja, na anapogeuka, mnamfanya astahili Gehena^{*} mara mbili zaidi yenu.

16 “Ole wenu, viongozi vipofu^c mnaosema, ‘Yeyote akiapa kwa hekalu, si kitu; lakini yeyote akiapa kwa dhahabu ya hekalu, yuko chini ya wajibu.’^d **17** Wapumbavu na vipofu! Kwa kweli, ni kipi kilicho kikubwa zaidi, dhahabu au hekalu linaloitakasa dhahabu hiyo? **18** Isitoshe, ‘Yeyote akiapa kwa madhabahu, si kitu; lakini yeyote akiapa kwa zawadi iliyo kwenye madhabahu, yuko chini ya wajibu.’ **19** Ninyi vipofu! Kwa kweli, ni kipi kilicho kikubwa zaidi, zawadi au madhabahu ambayo huitakasa zawadi hiyo? **20** Kwa hiyo yeyote anayeapa kwa madhabahu anaapa kwa madhabahu na kwa kila kitu kilicho juu yake; **21** na yeyote anayeapa kwa hekalu anaapa kwa hekalu na kwa Yule anayekaa ndani yake;^e **22** na yeyote anayeapa kwa mbingu anaapa kwa kiti cha ufalme cha Mungu na kwa Yule anayeketi juu yake.

23 “Ole wenu, waandishi na Mafarisayo wanafiki! kwa sababu mnatoa sehemu ya kumi ya mnanaa na dili na bizari,^f lakini mmepuuzi mambo mazito zaidi ya Sheria, yaa-ni, haki,^g rehema,^h na uamini-fu. Mlipaswa kufanya mambo

23:14 *Angalia Nyongeza A3. 23:15 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

hayo, bila kupuuzia yale mengine.^a **24** Viongozi vipofu,^b ambao huchuja mbu^c lakini hummeza ngamia!^d

25 “Ole wenu, waandishi na Mafarisayo wanafiki! kwa sababu mnasafisha upande wa nje wa kikombe na wa sahani,^e lakini ndani vimejaa pupa^{*f} na kutojizuia.^g **26** Farisayo kipofu, safisha kwanza ndani ya kikombe na sahani ili upande wa nje uwe safi pia.

27 “Ole wenu, waandishi na Mafarisayo wanafiki!^h kwa sababu mnafanana na makaburi yaliyopakwa chokaa,ⁱ ambayo kwa nje yanapendeza lakini ndani yamejaa mifupa ya wafu na kila namna ya ucha-fu. **28** Vivyo hivyo, kwa nje mnaonekana waadilifu kwa watu, lakini ndani mmejaa unafiki na uasi sheria.^j

29 “Ole wenu, waandishi na Mafarisayo wanafiki!^k kwa sababu mnajenga makaburi ya manabii na kuyarembe-sha makaburi* ya waadilifu,^l **30** nanyi mnasema, ‘Kama tungeishi katika siku za mababu zetu, hatungeshirikiana nao kumwaga damu ya manabii.’ **31** Kwa hiyo, mnashuhudia dhidi yenu wenyewe kwamba ninyi ni wana wa wale waliowaua manabii.^m **32** Basi, kijazeni kipimo cha mababu zenu.

33 “Ninyi nyoka, wana wa nyoka,^{*n} mtaikimbiaje hukumu ya Gehena?^o **34** Kwa sababu hiyo, ninawatuma kwenye manabii^p na watu wenye hekima na walimu wa watu

23:25 *Au “vitu vilivyoporwa.” 23:29 *Au “makaburi ya ukumbusho.” 23:33 *Au “nyoka-vipiri.” ^aAngalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 23

a Lu 11:42

b Mt 15:14

c Law 11:23

d Lu 11:4

e Mk 7:3, 4

f Mk 12:38, 40

g Lu 11:39

h Lu 12:56

i Lu 11:44

Mdo 23:3

j Lu 16:15

k Mt 6:2

l Lu 11:47

m Lu 11:48

Mdo 7:52

Ebr 11:32, 37

n Mt 3:7

Mt 12:34

Lu 3:7

o Mt 10:28

Lu 12:5

p Lu 11:49-51

Safu ya 2

a Mt 13:52

b Yoh 16:2

Mdo 7:59

c Mdo 5:40

2Ko 11:24

d Lu 21:12

e Mwa 4:8, 10

Ebr 11:4

f 2Nya 24:20-22

g Yoh 8:59

Ebr 11:32, 37

h Lu 13:34

Lu 19:41, 42

i 1Fa 9:7, 8

Yer 12:7

Yer 22:5

Mt 21:43

Lu 21:20

j Zb 118:26

SURA YA 24

k Mk 13:1, 2

Lu 19:44

Lu 21:5, 6

wote.^a Baadhi yao mtawaua^b na kuwatundika kwenye miti, na baadhi yao mtawapiga mi-jeledi^c katika masinagogi yenu na kuwatesa^d katika jiji baada ya jiji, **35** ili damu yote ya waadilifu iliyomwagwa dunia-ni ije juu yenu, kuanzia damu ya Abeli^e mwadilifu mpaka damu ya Zekaria mwana wa Barakia, ambaye mlimuua kati ya patakifu na madhabahu.^f **36** Kwa kweli ninawaambia, mambo yote haya yatakipata kizazi hiki.

37 “Yerusalemu, Yerusalemu, muuaji wa manabii na aliyewapiga mawe wale waliotumwaga kwake^g—nilijaribu mara ngapi kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku anavyokusanya vifaranga wake chini ya mabawa yake! Lakini hamkutaka.^h **38** Tazama! Mmeachiwa nyumba yenu.^{*i}

39 Kwa maana ninawaambia, tangu sasa hamtaniona tena mpaka mtakaposema, ‘Amebarikiwa yule anayekuja katika jina la Yehova!’^{*j}

24 Yesu alipokuwa akito-ka hekaluni, wanafunzi wake wakamkaribia na kumwonyesha majengo ya hekalu. **2** Akawaambia: “Je, mnaona vitu hivi vyote? Kwa kweli ninawaambia, hakuna jiwe litakaloachwa hapa juu ya jiwe lingine bila kuangushwa chini.”^k

3 Alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wakamkaribia faraghani, wakamuuliza: “Tuambie, mambo haya yatatukia lini, na ni nini itakayokuwa ishara ya

23:38 *Au labda, “Mmeachiwa nyumba yenu ukiwa.” 23:39 *Angalia Nyo-geza A5.

kuwapo*^a kwako na ya umalizio wa mfumo wa mambo?"^{*b}

4 Yesu akawajibu: "Jihadharini ili mtu yeyote asiwapotoshe,^c **5** kwa maana wengi watakuja kwa msingi wa jina langu, wakisema, 'Mimi ndiye Kristo,' nao watawapotosha wengi.^d **6** Mtasikia kuhusu vita na habari za vita. Msishtuke kwa maana lazima mambo hayo yatukie, lakini ule mwisho bado.^e

7 "Kwa maana taifa litipigana na taifa na ufalme kupigana na ufalme,^f kutakuwa na upungufu wa chakula^g na matetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali.^h **8** Mambo hayo yote ni mwanzo wa maumivu ya taabu.

9 "Kisha watu watawakabidhi kwenye dhiki' na kuwau ninyi,ⁱ nanyi mtachukiwa na mataifa yote kwa sababu ya jina langu.^k **10** Pia, wengi watakwazika, nao watasalitiana na kuchukiana. **11** Manabii wengi wa uwongo watatokea na kuwapotosha wengi;^j **12** na kwa sababu ya kuongezeka kwa uasi sheria, upendo wa wengi utapoa. **13** Lakini yule atakayevumilia* mpaka mwisho ndiye atakayeokolewa.^m **14** Na hii habari nje-ma ya Ufalme itahubiriwa katika dunia yote inayokaliwa ili kuwa ushahidi kwa mataifa yote,ⁿ na ndipo ule mwisho utakapokuja.

15 "Kwa hiyo, mtakapoo-na kile kitu chenye kuchukiza sana kinachosababisha ukiwa, kama alivyosema nabii Danieli, kikiwa kimesimama mahali patakatifu^o

24:3, 27 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 24:13 *Au "anayevumilia."

SURA YA 24

a Mt 24:27
Mt 24:37-39
b Mt 13:39
Mt 28:20
Mk 13:3, 4
Lu 21:7
c Mk 13:5, 6
Lu 21:8
d Mt 24:24
e Mk 13:7
Lu 21:9
f Ufu 6:4
g Mdo 11:28
Ufu 6:6
h Mk 13:8
Lu 21:10, 11
i Yoh 15:20
Mdo 11:19
Ufu 2:10
j Yoh 16:2
Mdo 7:59
Mdo 12:1, 2
Ufu 6:11
k Mt 10:17, 22
Mk 13:9, 13
Lu 21:12, 13
Lu 21:17
Yoh 15:21
2Ti 3:12
l Mt 7:15
1Ti 4:1
2Pe 2:1
m Mt 10:22
Mk 13:13
Lu 21:19
Ebr 10:36
n Mt 9:35
Mt 28:19, 20
Mk 13:10
Ufu 14:6
o Da 9:27
Da 11:31
Da 12:11
Mk 13:14-18
Lu 21:20

Safu ya 2

a Lu 21:21-23
b Lu 21:23
Ufu 7:14
c Da 12:1
Mk 13:19
d Mk 13:20
e Mt 24:5
f Mk 13:21-23
g Mt 7:15
2Pe 2:1
h Mt 7:22, 23
2Th 2:9
i Lu 17:23
j Lu 17:24
k Lu 17:37

(msomaji na atumie utambu-zi), **16** ndipo wale walio Yudea waanze kukimbilia milimani.^a **17** Mtu aliye juu ya paa la nyumba asishuke kuchukua mali ndani ya nyumba yake; **18** na mtu aliye shambani asirudi kuchukua vazi lake la nje. **19** Ole wao wanawake wenye mimba na wale wanaonyonyesha mtoto katika siku hizo! **20** Endeeleni kusali ili mtakapokimbia isive wakati wa majira ya bari-di kali wala siku ya Sabato; **21** kwa maana wakati huo kutakuwa na dhiki kuu^b ambayo haijawahi kutokea tangu mwanzo wa ulimwengu mpaka sasa, hapana, wala haitatokea tena.^c **22** Kwa kweli, kama siku hizo hazingefupishwa, hakuna mwili wowote ambao ungeokolewa; lakini kwa sababu ya wale waliochaguliwa, siku hizo zitafupishwa.^d

23 "Na ikiwa mtu yeyote atawaambia, 'Tazama! Kristo yuko hapa,'^e au, 'Yuko pale!' msiamini.^f **24** Kwa maana Kristo wengi wa uwongo na manabii wa uwongo^g watatokea na kufanya ishara kubwa na maajabu ili kuwapotosha,^h ikiwezekana, hata wale waliochaguliwa. **25** Tazama! Ni-mewaonya mapema. **26** Basi, watu wakiwaambia, 'Tazama! Yuko nyikani,' msiende; 'Tazama! Yumo katika vyumba vya ndani,' msiamini.ⁱ **27** Kwa maana kama radi inavyotokea mashariki na kuangaza mpaka magharibi, ndivyo kuwapo* kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa.^j **28** Popote palipo na mzoga, hapo ndipo tai watakapokusan-nyika.^k

29 “Mara tu baada ya dhiki ya siku hizo jua litatiwa giza,^a mwezi hautatoa nuru yake, nyota zitaanguka kutoka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikiswa.^b 30 Ndipo ishara ya Mwana wa binadamu itakapoonekana mbinguni, na makabila yote ya dunia yatajipigapiga kwa huzuni,^c nayo yatamwona Mwana wa binadamu^d akija juu ya mawingu ya mbinguni akiwa na nguvu na utukufu mwingi.^e 31 Kisha atawatuma malaika zake pamoja na sauti kubwa ya tarumbeta, nao watawakusanya watu wake waliochaguliwa kutoka kwenye zile pepo nne za dunia, kuanzia mwisho mmoja wa mbingu mpaka mwisho mwingine.^f

32 “Basi jifunzeni mfano huu kutokana na mtini: Mara tu matawi yake machanga yanapokuwa laini na kuchipua majani, mnajua kwamba kiangazi kinakaribia.^g 33 Vivyo hivyo, ninyi pia mtakapoona mambo yote hayo, jueni kwamba yuko karibu milangoni.^h 34 Kwa kweli ninawaambia kizazi hiki hakitapitilia mbali kamwe mpaka mambo haya yote yatukie. 35 Mbingu na dunia zitapitilia mbali, lakini maneno yangu hayatapitilia mbali kamwe.ⁱ

36 “Kuhusu siku hiyo na saa hiyo, hakuna mtu anayejua,^j hata malaika wa mbinguni wala Mwana, ila Baba tu.^k 37 Kwa maana kama siku za Noa zilivyokuwa,^l ndivyo kuwapo* kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa.^m 38 Kwa maana kama walivyokuwa katika siku hizo kab-

SURA YA 24

a Yoe 2:31

b Mk 13:24, 25
Lu 21:25, 26

c Ufu 1:7

d Da 7:13

e Mt 26:64
Mk 13:26
Lu 21:27

f Mk 13:27

g Mk 13:28-31
Lu 21:29-33

h Yak 5:8, 9

i Lu 21:33

j 1Th 5:1, 2

k Mk 13:32
Mdo 1:7

l Mwa 6:11-13

m Lu 17:26, 27

Safu ya 2

a Mwa 7:7
Ebr 11:7
1Pe 3:19, 20
2Pe 2:5b Mwa 7:23
2Pe 3:6

c Lu 17:35

d Mt 25:13
Mk 13:33
Lu 21:36e 1Th 5:2
2Pe 3:10

f Lu 12:39, 40

g Mk 13:35

h Lu 12:42-44

i Ufu 16:15

j Lu 12:45, 46

la ya Gharika, wakila na kunywa, wanaume wakioa na wanawake wakiolewa, mpaka siku ambayo Noa alingia ndani ya safina,^a 39 nao hawakujali mpaka Gharika ikaja na kuwafagilia mbali wote,^b ndivyo kuwapo kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa. 40 Kisha wanaume wawili watakuwa shambani; mmoja atachukuliwa na mwingine ataa-chwa. 41 Wanawake wawili watakuwa wakisaga kwenye jiwe la kusagia; mmoja atachukuliwa na mwingine ataa-chwa.^c 42 Kwa hiyo, endeleeni kukesha kwa sababu hamjui Bwana wenu atakuja siku gani.^d

43 “Lakini jueni jambo hili: Ikiwa mwenye nyumba angejua mwizi atakuja katika kesho gani,^e angekaa macho na hangeruhusu nyumba yake ivunjwe.^f 44 Kwa hiyo ninyi pia iweni tayari,^g kwa sababu Mwana wa binadamu atakuja saa msiyotazamia.

45 “Kwa kweli ni nani mtumwa mwaminifu na mwenye busara* ambaye bwana wake alimweka rasmi asimamie watumishi wake wa nyumbani na kuwapa chakula chao kwa wakati unaofaa?^h 46 Mwenye furaha ni mtumwa huyo ikiwa bwana wake atakapokuja atamkuta akifanya hivyo!ⁱ 47 Kwa kweli ninawaambia, atamweka rasmi asimamie mali zake zote.

48 “Lakini ikiwa mtumwa huyo mwovu atasema moyoni mwake, ‘Bwana wangu anakawia,’^j 49 naye aanze kuwapi-ga watumwa wenzake na kula na kunywa pamoja na wale-

24:43 *Au “wakati gani wa usiku.”

24:45 *Au “hekima.”

vi wa kupindukia, **50** bwana wa mtumwa huyo atakuja siku asiyotazamia na katika saa asiyojua,^a **51** naye atamwadhibu kwa ukali sana na ku-mweka pamoja na wanafiki. Huko ndiko atalia na kusaga meno yake.^b

25 “Basi Ufalme wa mbinguni ni kama mabikira kumi waliochukua taa zao^c na kwenda kumpokea bwana harusi.^d **2** Watano kati yao walikuwa wapumbavu, na watano walikuwa wenye busara.*^e **3** Wale wapumbavu walibeba taa zao lakini hawakubeba mafuta, **4** lakini wale wenye busara walibeba mafuta kwenye chupa zao pamoja na taa zao. **5** Bwana harusi alipokawia kuja, wote walisinzia na kulala. **6** Katikati ya usiku kukatokea mwito, ‘Huyu hapa Bwana harusi! Nendeni mkamlaki.’ **7** Ndi-po mabikira wote wakasimama na kuzitayarisha taa zao.^f **8** Wale wapumbavu wakawambia wenye busara, ‘Tugawieni mafuta yenu, kwa sababu taa zetu zinakaribia kuzimika.’ **9** Wale wenye busara wakawajibu: ‘Labda hayatatutosha sisi sote. Nendeni kwa wauzaji mkajinunulie.’ **10** Walipokuwa wakienda kununua mafuta, bwana harusi akaja. Mabikira waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye kwenye karamu ya ndoa,^g na mlango ukafungwa. **11** Baadaye wale mabikira wengine pia wakaja, wakisema, ‘Bwana, Bwana, tufungulie!’^h **12** Akawajibu, ‘Kwa kweli ninawaambia, siwajui ninyi.’

25:2 *Au “hekima.”

SURA YA 24

a Mt 25:13

b Mt 13:42

SURA YA 25

c Lu 12:35

Flp 2:15

d Yoh 3:28, 29

Ufu 19:7

e Mt 7:24, 26

f Lu 12:35

g Ufu 19:9

h Lu 13:25, 27

Safu ya 2

a 1Th 5:6

1Pe 5:8

b Mt 24:42, 50

Mk 13:33

c Lu 19:12, 13

d Lu 19:15

e Lu 19:16, 17

f Lu 16:10

g Ebr 12:2

h Lu 19:18, 19

13 “Kwa hiyo, endeleeni ku-kesha^a kwa sababu hamjui ile siku wala saa.^b

14 “Kwa maana ni kama mtu aliye karibu kusafiri ng’ambo, aliyewaita watumwa wake na kuwakabidhi mali zake.^c **15** Akampa mmoja talanta* tano, mwingine mbili, na mwingine moja, kila mtumwa kulingana na uwezo wake, kisha akaenda ng’ambo. **16** Mara moja yule aliyepokea talanta tano akaenda kufanya biashara nazo, akapata talanta tano zaidi. **17** Vivyo hivyo, yule aliyepokea mbili akapata talanta mbili zaidi. **18** Lakini mtumwa aliyepokea moja tu akaenda akachimba shimo ardhini na kuficha zile pesa* za bwana wake.

19 “Baada ya muda mrefu, bwana wa watumwa hao akarudi na kufanya hesabu nao.^d **20** Basi, yule aliyepokea talanta tano akaja na kuleta talanta tano zaidi, akisema, ‘Bwana, ulinikabidhi talanta tano, ona, nimepata talanta tano zaidi.’^e **21** Bwana wake akamwambia: ‘Vema, mtumwa mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu katika mambo machache. Nita-kuweka juu ya mambo mengi.’^f Ingia katika shangwe ya bwana wako.^g **22** Kisha yule aliyepokea talanta mbili akaja na kusema, ‘Bwana, ulinikabidhi talanta mbili, ona, nimepata talanta mbili zaidi.’^h **23** Bwana wake akamwambia: ‘Vema, mtumwa mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu katika mambo machache. Nitakuweka juu ya mambo mengi.’

25:15 *Talanta ya Wagiriki ilikuwa sawa na kilogramu 20.4. Angalia Nyongeza B14. 25:18 *Tnn., “fedha.”

Ingia katika shangwe ya bwana wako.'

24 "Mwishowe mtumwa aliyepokea talanta moja akaja na kusema: 'Bwana nilijua wewe ni mtu mgumu, ambaye huvuna mahali ambapo hukupanda na kukusanya mahali ambapo hukupepeta.^a **25** Kwa hiyo, niliogopa nikaenda na kuficha talanta yako ardhini. Chukua mali yako.' **26** Bwana wake akamjibu: 'Mtumwa mwovu na mvivu, ulijua kwamba nilivuna mahali ambapo sikupanda na kukusanya mahali ambapo sikupepeta, sivyo? **27** Basi, ungeweka pesa* zangu benki, ili nitakaporudi nizichukue pamoja na faida.

28 "Kwa hiyo, ichukueni talanta hiyo kutoka kwake mkampe yule mwenye talanta kumi.^b **29** Kwa maana kila mtu aliye na kitu ataongezea, naye atakuwa na vitu vingi. Lakini mtu asiye na kitu, hata kile alichu nacho kitachukuliwa.^c **30** Basi mtupeni nje gizani mtumwa huyo asiyefaa kitu. Huko ndiko atalia na kusaga meno yake.'

31 "Mwana wa binadamu^d atakapokuja katika utukufu wake, pamoja na malaika wote,^e ataketi kwenye kiti chake cha ufalme chenye utukufu. **32** Mataifa yote yatakusanyika mbele yake, naye atawatenganisha watu mmoja kutoka kwa mwenzake, kama vile mchungaji anavyotenganisha kondoo na mbuzi. **33** Naye atawaweka kondoo^f kwenye mkono wake wa kuumu, lakini mbuzi kwenye mkono wake wa kushoto.^g

25:27 * Tnn., "fedha."

SURA YA 25

a Lu 19:20-23

b Lu 19:24-26

c Mt 13:12
Mk 4:25
Lu 8:18
Yoh 15:2

d Da 7:13

e Mt 16:27

f Yoh 10:14

g Mt 25:41

Safu ya 2

a Ebr 13:2
3Yo 5

b Yak 2:15, 16

c ZTi 1:16

d Mt 10:42

e Met 19:17
Mt 10:40
Mk 9:41
Ebr 6:10

f Mt 7:23

g Mt 18:8, 9

h Ufu 12:9
Ufu 20:10

34 "Ndipo Mfalme atawaaambia wale walio kwenye mkono wake wa kuumu: 'Njoo ni, ninyi ambao mmebarikiwa na Baba yangu, urithini Ufalme uliotayarishwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu. **35** Kwa maana nilikuwa na njaa mkani-pa chakula; nilikuwa na kiu mkanipa kinywaji. Nilikuwa mgeni mkanikaribisha vizuri;^a **36** nilikuwa uchi,^{*} mkanivika nguo.^b Nilikuwa mgonjwa mkanitunza. Nilikuwa gerezani mkanitembelea.'^c **37** Ndipo waadilifu watamuuliza: 'Bwana, ni lini tulipokuona ukiwa na njaa tukakulisha, au ukiwa na kiu tukakupa kinywaji?^d **38** Ni lini tulipokuona ukiwa mgeni tukakukaribisha, au ukiwa uchi tukakuvika? **39** Ni lini tulipokuona ukiwa mgonjwa au ukiwa gerezani tukakutembelea?' **40** Mfalme atawajibu, 'Kwa kweli ninawaambia, kwa kadir ambavyo mlimtendea aliye mdogo zaidi kati ya hawa ndugu zangu, mlinitendea mimi.'^e

41 "Kisha atawaambia wale walio kwenye mkono wake wa kushoto: 'Ondokeni kwangu^f ninyi mliolaaniwa, nendeni katika moto wa milele^g aliotayarishiwa Ibilisi na malaika zake.^h **42** Kwa maana nilikuwa na njaa, lakini hamkunipa chakula, nilikuwa na kiu, lakini hamkunipa kinywaji. **43** Nilikuwa mgeni, lakini hamkunikaribisha; nilikuwa uchi, lakini hamkunivika nguo; nilikuwa mgonjwa na nilikuwa gerezani lakini hamkunitunza.' **44** Nao pia watamuuliza: 'Bwana, ni lini tu-

25:36 * Au "sikuwa na mavazi ya kutosha."

lipokuona ukiwa na njaa au ukiwa na kiu au ukiwa mgeni au ukiwa uchi au ukiwa mgonjwa au ukiwa gerezani tukakosa kukuhudumia? **45** Ndiipo atawajibu: 'Kwa kweli ninawaambia, kwa kadiri ambavyo hamkumtendea mmoja wa hawa wadogo zaidi, hamkunitendea mimi.'^a **46** Hao watakatiliwa mbali milele,^{*b} lakini waadilifu watapata uzima wa milele."^c

26 Basi Yesu alipomaliza kusema hayo yote, akawaambia wanafunzi wake: **2** "Mnajua kwamba baada ya siku mbili kutakuwa na Pasaka,^d naye Mwana wa binadamu atatolewa ili auawe kwenye mti."^e

3 Ndipo wakuu wa makuhani na wazee wa watu wakakusanyika katika ua wa kuhani mkuu aliyetwa Kayafa,^f **4** nao wakapanga njama pamoja^g ili kumkamata Yesu kwa hila* na kumuua. **5** Hata hivyo, walikuwa wakisema: "Si kwenye sherehe, ili watu wasifanye ghasia."

6 Yesu alipokuwa Bethania katika nyumba ya Simoni mwenye ukoma,^h **7** mwana mke fulani aliyekuwa na chupa ya alabasta yenye mafuta ghali yenye marashi akamkaribia, akaanza kuyamimina juu ya kichwa cha Yesu alipokuwa akila.* **8** Walipoona hilo wanafunzi wakakasirika na kusema: "Hasara hii ni ya nini? **9** Kwa maana mafuta haya yangeuzwa kwa kiasi kikubwa cha pesa na kupewa maskini." **10** Akijua jambo hilo, Yesu

25:46 *Yaani, kutoka kwa uhaj. Tnn., "kukata matawi; kupogolewa." **26:4** *Au "kwa ujanja." **26:7** *Au "alipokuwa ameketi mezani."

SURA YA 25

- a Zek 2:8
Mdo 9:4, 5
b 2Pe 2:9
c Ro 2:6, 7

SURA YA 26

- d Kut 12:14
Mk 14:1, 2
Lu 22:1, 2
Yoh 13:1
e Mt 16:21
Mt 20:18, 19
Mt 27:26
Mk 15:15
Yoh 19:16
f Mt 26:57
Lu 3:2
Yoh 11:49
Yoh 18:13, 24
g Zb 2:2
h Mk 14:3-9
Yoh 12:1-8

Safu ya 2

- a Kum 15:11
b Mk 14:7
c Mk 14:8
Yoh 12:7
d Mk 14:9
e Mt 10:2, 4
Yoh 13:2
f Mk 14:10, 11
Lu 22:3-6
g Yoh 11:57
h Kut 21:32
Zek 11:12
Mt 27:3
i Kut 12:18
Kut 23:15
Lu 22:1
j Mk 14:12-16
Lu 22:7-13
k Kum 16:6

- l Mk 14:17-21
Lu 22:14
m Lu 22:21-23
Yoh 6:70
Yoh 13:21, 22

akawaambia: "Kwa nini mnataka kumsumbua mwanamke huyu? Amenitendea jambo jema. **11** Kwa maana maskini mnao sikuzote,^a lakini mimi hamtakuwa nami sikuzote.^b **12** Alipomimina mafuta haya yenye marashi kwenye mwili wangu, alifanya hivyo ili kunitayarisha kwa ajili ya mazishi.^c **13** Kwa kweli ninawaambia, popote ambapo hii habari nje-ma itahubiriwa ulimwenguni, jambo alilofanya mwanamke huyu litatajwa pia ili kumkumbuka."^d

14 Ndipo mmoja wa wale 12, aliyetwa Yuda Iskariote,^e akaenda kwa wakuu wa makuhani^f **15** na kuwauliza: "Mtanipa nini ili nimsaliti kwenye?"^g Wakakubaliana naye vipande 30 vya fedha.^h **16** Basi tangu wakati huo akaanza kutafuta nafasi nzuri ya kumsaliti.

17 Siku ya kwanza ya Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachuⁱ wanafunzi wakaja kumuuliza Yesu: "Unataka tukutayarishie wapi mlo wa Pasaka?"^j **18** Akawaambia: "Nendeni jijini kwa mwanamume fulani mkamwambie, 'Mwali mu anasema: "Wakati wangu uliowekwa umekaribia; nitasherehekea Pasaka pamoja na wanafunzi wangu nyumbani kwako."^k **19** Basi, wanafunzi wakafanya kama Yesu alivyowaagiza, wakaandaa Pasaka.

20 Ilipofika jioni,^k Yesu alikuwa ameketi mezani pamoja na wale wanafunzi 12.^l **21** Walipokuwa wakila, akasema: "Kwa kweli ninawaambia, mmoja wenu atanisaliti."^m **22** Wakiwa wamehuzunishwa sana na jambo hilo,

kila mmoja wao akaanza kumuuliza: “Bwana, je, ni mimi?”

23 Akawajibu: “Anayechovya mkono wake pamoja nami katika bakuli ndiye atakayenisaliti.^a **24** Kwa kweli, Mwana wa binadamu anaenda zake, kama ilivyoandikwa kumhusu, lakini ole^b wake mtu atakayemsaliti Mwana wa binadamu!^c Ingekuwa afadhali kama mtu huyo hangezaliwa.”^d **25** Yuda, aliyekuwa karibu kumsaliti akauliza: “Je, ni mimi, Rabi?” Yesu akamjibu: “Wewe mwenyewe ume-sema.”

26 Walipokuwa wakiendelea kula, Yesu akachukua mkate, na baada ya kutoa baraka, akaumege,^e akawapa wanafunzi wake, akasema: “Chukueni mle. Huu unamaanisha mwili wangu.”^f **27** Kisha akachukua kikombe, akashukuru na kuwapa akisema: “Kunyweni ninyi nyote,^g **28** kwa maana hii inamaanisha ‘damu yangu^h ya agano,ⁱ ambayo itamwagwa kwa ajili ya wengi^j ili wasamehe wame dhambi.^k **29** Lakini ninawaambia: sitakunywa tena kamwe divai yoyote ya mzabibu mpaka siku nitakapoinywa ikiwa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba yangu.”^l **30** Mwishowe, baada ya kuimba sifa,^m wakaenda kwenye Mlima wa Mizeituni.^m

31 Ndipo Yesu akawaambia: “Ninyi nyote mtakwazika kuhusiana nami usiku wa leo, kwa maana imeandikwa: ‘Nitampiga mchungaji, nao kondoo wa kundi watatawanyika.’ⁿ **32** Lakini baada ya kufufuliwa nitawatangulia kui-

SURA YA 26

a Zb 41:9
Mk 14:20
Lu 22:21
Yoh 13:26
b Kum 27:25
c Lu 22:22
Yoh 17:12
d Mk 14:21
e 1Ko 10:16
f Mk 14:22
Lu 22:19
1Ko 11:23-26
g Mk 14:23
Lu 22:20
h 1Ko 10:16
i Kut 24:8
Yer 31:31
Ebr 7:22
j Mt 20:28
Mk 14:24
k Efe 1:7
Ebr 9:20, 22
l Mk 14:25
Lu 22:18
m Lu 22:39
Yoh 18:1
n Zek 13:7
Mk 14:27, 28
Yoh 16:32

Safu ya 2

a Mt 28:7
Mt 28:16
b Mk 14:29-31
c Mk 14:30
Lu 22:34
Yoh 13:38
d Lu 22:33
e Yoh 18:1
f Mk 14:32-36
Lu 22:40
g Isa 53:3
h Mk 14:34
i Ebr 5:7
j Mt 20:22
Yoh 18:11
k Mk 14:36
Lu 22:42
Yoh 5:30
Yoh 6:38
Ebr 10:9
l Mk 14:37-42
Lu 22:45
m Mk 13:33
1Pe 5:8
Ufu 16:15
n Lu 18:1
Ro 12:12
Efe 6:18
1Pe 4:7
o Mt 6:13
Lu 22:46
p Mk 14:38
Ro 7:23

ngia Galilaya.”^a **33** Lakini Petro akajibu: “Hata wengine wote wakikwazika kuhusiana nawe, mimi sitakwazika kamwe!”^b **34** Yesu akamwambia: “Kwa kweli ninakuambia, usiku huu, kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu.”^c **35** Petro akamwambia: “Hata nikilazimika kufa pamoja nawe, sitakukana kamwe.”^d Wale wanafunzi wengine wote wakasema vi-vyo hivyo.

36 Ndipo Yesu akaja pamoja nao mpaka mahali panapoitwa Gethsemane,^e akawaambia wanafunzi: “Ketini hapa, mimi naenda pale kusali.”^f **37** Akamchukua Petro na wale wana wawili wa Zebedayo, naye akaanza kuhuzunika na kutaabika sana.^g **38** Ndipo akawaambia: “Nimehuzunika* sana, kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mwendeleo kukesha pamoja nami.”^h **39** Akasonga mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akasali: “Baba yangu, ikiwa inawezekana, niondolee kikombe hiki.ⁱ Lakini, si kama ninavyopenda, bali kama unavyopenda.”^k

40 Akarudi na kuwakuta wanafunzi wakiwa wamela-la usingizi, akamuuliza Petro: “Je, hamngeweza kukesha pamoja nami hata kwa saa moja?^l **41** Endeleei kukesha^m na kusali bila kucha,ⁿ ili msiingie katika majaribu.^o Bila shaka, roho inataku* lakini mwili ni dhaifu.”^p **42** Akaenda tena mara ya pili na kusali: “Baba yangu, ikiwa siwezi kuepuka kunywa

26:38 *Au “nafsi yangu inahuzunika.”
26:41 *Au “inapenda.”

kikombe hiki, acha mapenzi yako yatendeke.”^a **43** Akaja tena na kuwakuta wakiwa wamelala usingizi, kwa maana macho yao yalikuwa mazito. **44** Basi akawaacha, akaenda tena kusali mara ya tatu, aki-sema tena jambo lilelile. **45** Kisha akarudi na kuwaambia wanafunzi: “Mnalala na kupumzika wakati kama huu! Tazama! Saa imekaribia ya Mwana wa binadamu kusalitiwa mikononi mwa watenda dhambi. **46** Simameni twnde. Tazama! Msaliti wangu amekaribia.” **47** Alipokuwa bado akizungumza, tazama! Yuda, mmoja wa wale 12, akaja pamoja na umati mkubwa wakiwa na mapanga na marungu, walikuwa wametumwa na wakuu wa makuhani na wazee wa watu.^b

48 Basi msaliti wake alikuwa amewapa ishara, aki-sema: “Yule nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni.” **49** Akaenda moja kwa moja kwa Yesu akasema: “Salamu, Rabi!” kisha akambusu kwa wororo. **50** Lakini Yesu akamuuliza: “Mwenzangu, ume-kuja kufanya nini?”^c Ndipo wakaja na kumkamata Yesu na kumtia nguvuni. **51** Lakini tazama! mmoja wa wale waliokuwa pamoja na Yesu akanyoosha mkono wake, akauchomoa upanga wake, akampiga mtumwa wa kuhani mkuu na kumkata sikio.^d **52** Ndipo Yesu akamwambia: “Rudisha upanga wako mahali pake,^e kwa maana wote wanaochukua upanga wataangamia kwa upanga.^f **53** Au unafikiri siwezi kumwomba Baba yangu anipe sasa hivi vikosi zaidi ya

SURA YA 26

a Mt 6:10
Yoh 12:27

b Mk 14:43-47
Lu 22:47-51
Yoh 18:3

c Zb 41:9

d Mk 14:47
Lu 22:50
Yoh 18:10

e Yoh 18:11

f Mwa 9:6

Safu ya 2

a 2Fa 6:17
Da 7:10
Mt 4:11

b Lu 19:47
Yoh 18:20

c Mk 14:48, 49
Lu 22:52, 53

d Zb 22:16-18
Isa 53
Da 9:26

e Zek 13:7
Mk 14:50
Yoh 16:32

f Yoh 18:13

g Mk 14:53, 54
Lu 22:54, 55

h Yoh 18:16

i Mk 14:55-59

j Zb 27:12
Zb 35:11

k Mt 27:39, 40
Yoh 2:19
Mdo 6:14

l Mk 14:60-65

m Isa 53:7
Mdo 8:32

12 vya malaika?^a **54** Hata hivyo, Maandiko yanayosema lazima itendeke hivi yatatimizwaje?” **55** Saa hiyo, Yesu akauambia umati: “Je, mme-kuja kunikamata mkiwa na mapanga na marungu kana kwamba mimi ni mwizi? Siku baada ya siku nilikuwa nikiketihikaluni nikifundisha^b lakini hamkunikamata.^c **56** Lakini yote haya yametokea ili kutimiza mambo yaliyoandikwa* na manabii.”^d Ndipo wanafunzi wote wakamwacha na kukimbia.^e

57 Wale waliomkamata Yesu wakampeleka kwa Kayafa^f kuhani mkuu, ambako waandishi na wazee walikuwa wamekusanyika.^g **58** Lakini Petro akaendelea kumfuata kwa mbali, mpaka katika ua wa kuhani mkuu, na baada ya kuingia ndani, akaketi pamoja na watumishi wa nyumbani ili aone itakavyokuwa.^h

59 Sasa wakuu wa makuhani na Sanhedrini yote walikuwa wakitafuta ushahidi wa uwongo dhidi ya Yesu ili wamuue.ⁱ **60** Lakini hawakupata, ingawa mashahidi wengi wa uwongo walijitokeza.^j Baadaye, mashahidi wawili wakajitokeza **61** na kusema: “Mtu huyu alisema, ‘Nina-weza kuliangusha chini hekalu la Mungu na kulijenga kwa siku tatu.’”^k **62** Ndipo kuhani mkuu akasimama na kumuuliza: “Kwa nini hujibu? Watu hawa wanashuhudia nini kukuhusu?”^l **63** Lakini Yesu akakaa kimya.^m Basi kuhani mkuu akamwambia: “Ninakuapisha mbele za Mungu aliyehai utuambie kama

26:56 *Au “maandiko.”

wewe ndiye Kristo, Mwana wa Mungu!"^a **64** Yesu akamjibu: "Wewe mwenyewe umesema. Lakini ninawaambia: Tangu sasa mtamwona Mwana wa binadamu^b akiwa ameketi kwenye mkono wa kuume wa nguvu,^c akija juu ya mawingu ya mbinguni."^d **65** Ndipo kuhani mkuu akayararua mavazi yake ya nje, akisema: "Amekufuru! Tunahitaji mashahidi wengine wa nini? Tazama! Sasa mmemsikia akikufuru. **66** Mnaonaje?" Wakamjibu: "Anastahili kufa."^e **67** Kisha wakamtemea mate usoni^f na kumpiga ngumi.^g Wengine wakampiga makofi usoni,^h **68** wakisema: "Tutolee unabii, wewe Kristo. Ni nani aliyekupiga?"

69 Basi Petro alikuwa ameketi nje katika ua, kijakazi akamjia na kumwambia: "Hata wewe ulikuwa pamoja na Yesu Mgalilaya!"ⁱ **70** Lakini akakana mbele yao wote, akisema: "Sijui unachosema." **71** Alipoenda kwenye chumba kilicho langoni, msichana mwingine akamwona na kuwaambia wale waliokuwa hapo: "Mtu huyu alikuwa pamoja na Yesu Mnazareti."^j **72** Akakana tena akiapa: "Simjui mtu huyo!" **73** Baada ya muda mfupi wale waliokuwa wamesimama hapo wakaja na kumwambia Petro: "Hakika wewe pia ni mmoja wao, kwa maana matamshi* yako yanakutambuliha." **74** Ndipo akaanza kulaani na kuapa: "Simjui mtu huyo!" Na mara moja jogoo akawika. **75** Naye Petro akakumbuka maneno aliyosema Yesu, yaani: "Kabla jogoo ha-

26:73 *Au "lafudhi."

SURA YA 26

a Lu 22:67-71

b Da 7:13
Yoh 1:51

c Zb 110:1
Lu 22:69

d Mk 14:62
Ufu 1:7

e Law 24:16
Yoh 19:7

f Isa 50:6

g Lu 22:63, 64

h Isa 53:3

i Mk 14:66-72
Lu 22:54-62
Yoh 18:15-17

j Yoh 18:25-27

Safu ya 2

a Mt 26:34
Mk 14:30
Yoh 13:38

SURA YA 27

b Mk 15:1
Lu 22:66

c Zb 2:2
Mt 20:18, 19
Lu 23:1
Yoh 18:28
Mdo 3:13

d Mt 26:14, 15
Mk 14:10, 11

e Mdo 1:16, 18

f Mdo 1:19

g Zek 11:12, 13

jawika, utanikana mara tatu."^a Naye akaenda nje akalia kwa uchungu.

27 Ilipofika asubuhi, wakuu wote wa makuhani na wazee wa watu wakashauriana pamoja kumhusu Yesu ili auawe.^b **2** Baada ya kumfunga, wakampeleka na kumkabidhi kwa Pilato, gavana.^c

3 Ndipo Yuda, ambaye alimsaliti, alipoona Yesu amehukumiwa, akajuta na kuwarudishia wakuu wa makuhani na wazee vile vipande 30 vya fedha,^d **4** akisema: "Nilitenda dhambi niliposaliti damu isiyo na hatia." Wakamwambia: "Hilo linatuhusuje? Shauri yako!"^e **5** Basi akavitupa vile vipande vya fedha hekaluni. Kisha akaenda zake akajinyonga.^e **6** Lakini wakuu wa makuhani wakachukua pesa hizo wakasema: "Si halali kuziweka katika hazina takatifu, kwa sababu ni bei ya damu." **7** Baada ya kushauriana, wakatamia pesa hizo kununua shamba la mfinyanzi liwe mahali pa kuzika wageni. **8** Kwa hiyo, shamba hilo limeitwa Shamba la Damu^f hadi leo hii. **9** Ndipo yakatimia maneno haya yaliyosemwa kupitia nabii Yermia: "Nao wakavichukua vile vipande 30 vya fedha, bei iliyoamuliwa juu ya mtu huyo, ambaye bei yake iliamuliwa na baadhi ya wana wa Israeli, **10** nao wakavitoe ili kununua shamba la mfinyanzi, kama Yehova* alivyoniaturu."^g

11 Sasa Yesu akasimama mbele ya gavana, naye gavana akamuuliza: "Je, wewe ndiye

27:4 *Au "Utajua utakachofanya."

27:10 *Angalia Nyongeza A5.

Mfalme wa Wayahudi?" Yesu akajibu: "Wewe mwenyewe umesema."^a **12** Lakini alipokuwa akishtakiwa na wakuu wa makuhani na wazee, hakujibu.^b **13** Ndipo Pilato akamwambia: "Je, husikii ni mambo mangapi wanayoshuhudia dhidi yako?" **14** Lakini hakumjibu hata neno moja, hivi kwamba gavana akashangaa sana.

15 Sasa kila sherehe ya pasaka, gavana alikuwa na desturi ya kumfungua mfungwa yeyote ambaye umati ulimta-ka.^c **16** Wakati huo walikuwa wamemkamata mhalifu sugu aitwaye Baraba. **17** Basi walipokuwa wamekusanyika, Pilato akawauliza: "Mnataka niwafungulie nani, Baraba au Yesu anayeitwa Kristo?" **18** Kwa maana Pilato alijua kwamba walikuwa wamemkabidhi Yesu kwake kwa sababu ya wivu. **19** Zaidi ya hayo, alipokuwa ameketi kwenye kiti cha hukumu, mke wake akampelekea ujumbe huu: "Mwache mtu huyo mwadilifu, kwa maana niliteseka sana leo katika ndoto kwa sababu yake." **20** Lakini wakuu wa makuhani na wazee wakau-shawishi umati uombe Baraba afunguliwe,^d lakini Yesu auawe.^e **21** Gavana akawauliza: "Mnataka niwafungulie nani kati ya hawa wawili?" Wakasema: "Baraba." **22** Pilato akawaambia: "Basi, nifanye nini na Yesu anayeitwa Kristo?" Wote wakasema: "Atundikwe mtini!"^{*f} **23** Akawauliza: "Kwa nini? Amefanya kosa gani?" Wakaendelea kusema kwa sauti kubwa hata zaidi: "Atundikwe mtini!"^g

27:22 *Au "Auawe kwenye mti!"

SURA YA 27

a Mk 15:2-5
Lu 23:3
Yoh 18:33, 37

b Isa 53:7
Mt 26:63
Yoh 19:9

c Mk 15:6-10
Yoh 18:39

d Lu 23:18
Yoh 18:40
Mdo 3:14

e Mk 15:11-14

f Lu 23:21

g Lu 23:23
Mdo 3:13

Safu ya 2

a Mdo 5:27, 28
1Th 2:14, 15

b Lu 18:33
Yoh 19:1

c Mk 15:15
Lu 23:25

d Mk 15:16-20

e Yoh 19:2, 3

f Isa 50:6
Mt 26:67

g Isa 53:7
Mt 20:18, 19

h Mk 15:21
Lu 23:26

i Mk 15:22-24
Lu 23:33
Yoh 19:17

j Zb 69:21

24 Pilato alipoona jitihada zake hazifaulu, na bada-la yake ghasia zilikuwa zikito-kea, akachukua maji akanawa mikono mbele ya umati, akisema: "Mimi sina hatia ya damu ya mtu huyu. Shauri yenu." **25** Ndipo watu wote wakajibu: "Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu."^a **26** Ndipo akawafungulia Baraba, lakini akaagiza Yesu apigwe mijeledi^b na kumtoa ili auawe kwenye mti.^c

27 Ndipo wanajeshi wa gavana wakampeleka Yesu katika makao ya gavana, wakakusanya kikosi chote cha wanajeshi kumzunguka.^d **28** Wakamvua kanzu yake na kumvisha joho jekundu,^e **29** kisha wakasokota taji la miiba na kumvisha kichwani na kutia utete kwenye mkono wake wa kuume. Wakampigia magoti, wakamdhihaki wakisema: "Salamu,* ewe Mfalme wa Wayahudi!" **30** Wakamtemea mate^f na kuuchukua ule utete, wakaanza kumpiga kichwani. **31** Mwishowe, baada ya kumdhhihaki, wakamvua lile joho wakamvisha mavazi yake ya nje, wakampeleka akatundi-kwe mtini.^g

32 Walipokuwa wakitoka wakakutana na mwanamu-me kutoka Kirene aitwaye Simoni. Wakamlazimisha aubebe mti wa mateso^{*h} wa Yesu. **33** Na walipofika mahali panapoitwa *Golgotha*, yaani, Mahali pa Fuvu la Kichwa,ⁱ **34** wakampa divai iliyochanganywa na nyongo* anywe;^j lakini alipoionja, aka-kataa kuinywa. **35** Baada ya

27:29 *Au "Usifiwe." 27:32 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 27:34 *Kinywaji kichungu.

kumtundika kwenye mti, wakagawana mavazi yake ya nje kwa kupiga kura,^a **36** kisha wakaketi hapo wakimlinda. **37** Pia, wakabandika juu ya kichwa chake mashtaka dhidi yake, yalikuwa yameandikwa: “Huyu ni Yesu Mfalme wa Yahudi.”^b

38 Ndipo wezi wawili wakatundikwa kwenye mti kando yake, mmoja upande wake wa kuume na mwingine upande wake wa kushoto.^c **39** Na wale waliokuwa wakipita hapo wakamtukana,^d huku wakitikisa vichwa vyao^e **40** wakisema: “Wewe uliyetaka kuliangusha chini hekalu na kulijenga kwa siku tatu,^f jikoe mwenyewe! Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, shuka kutoka kwenye mti wa mateso!”^g **41** Vivyo hivyo, wakuu wa makuhani, waandishi, na wazee wakaaanza kumdhihaki wakisema:^h **42** “Aliwaokoa wengine lakini hawezi kujiokoa mwenyewe! Yeye ni Mfalme wa Israeli;ⁱ acheni sasa ashuke kutoka kwenye mti wa mateso* nasi tutamwamini. **43** Amemtegemea Mungu; acheni Mungu amwokoe ikiwa anamtaka,^j kwa maana alisema, ‘Mimi ni Mwana wa Mungu.’”^k **44** Vivyo hivyo, hata wezi waliotundikwa mtini kando yake walikuwa wakimshutumuni.^l

45 Kukawa na giza katika nchi yote kuanzia saa sita* mpaka saa tisa.^m **46** Karibu saa tisa, Yesu akapaza sauti, akisema: “*Eli, Eli, lama sabakhthani?*” yaani, “Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini

27:40, 42 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

27:45 *Yaani, karibu saa 6 mchana. ^aYaani, karibu saa 9 alasiri.

SURA YA 27

a Zb 22:18
Mk 15:24
Lu 23:34
Yoh 19:23, 24

b Mk 15:26
Lu 23:38
Yoh 19:19

c Isa 53:12
Mk 15:27
Lu 23:33
Yoh 19:18

d Lu 18:32
Ebr 12:3

e Zb 22:7
Lu 23:25

f Mt 26:60, 61
Yoh 2:19

g Mk 15:29-32

h Lu 23:35

i Yoh 1:49
Yoh 12:13

j Zb 22:8

k Mk 14:62
Yoh 5:18
Yoh 10:36

l Lu 23:39

m Mk 15:33
Lu 23:44

Safu ya 2

a Zb 22:1
Isa 53:10
Mk 15:34

b Mk 15:35, 36

c Zb 69:21
Lu 23:36
Yoh 19:29

d Mk 15:37
Lu 23:46
Yoh 19:30

e Kut 26:31-33
Ebr 9:3

f Ebr 10:19, 20

g Mk 15:38
Lu 23:45

h Mk 15:39

i Mk 15:40, 41
Lu 8:2, 3

j Mt 20:20
Yoh 19:25

umeniacha?”^a **47** Waliposikia hilo, baadhi ya wale walio kuwa wamesimama hapo wakaaanza kusema: “Mtu huyu anamwita Eliya.”^b **48** Mara moja, mmoja wao akakimbia, akachukua sifongo akailowesha katika divai kali akaiweka kwenye utete akampa anywe.^c **49** Lakini wengine wakasema: “Mwacheni! Acheni tunonekama Eliya atakuja kumwoko.”^d **50** Yesu akapaza tena sauti kisha akafa.^e^d

51 Na tazama! pazia la patakatifu^e likapasuka vipande viwili,^f kuanzia juu mpaka chini,^g dunia ikatetemeka, na miamba ikapasuka. **52** Makaburi* yakafunguka na miili mingi ya watakatifu waliokuwa wamelala usingizi ikainuliwa **53** (na watu waliokuwa wakitoka makaburini baada ya kufufuliwa kwake wakaingia katika jiji takatifu), nayo ikaoonwa na watu wengi. **54** Lakini yule ofisa wa jeshi na wale waliokuwa pamoja naye wakimlinda Yesu walipoona tete meko la ardhi na mambo yaliyokuwa yakitokea, wakaogopa sana na kusema: “Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu.”^h

55 Na wanawake wengi ambao walikuwa wamemfuata Yesu kutoka Galilaya ili kumhudumia walikuwa wakitazama kwa mbali;ⁱ **56** miongoni mwao kulikuwa na Maria Magdalene, Maria mama ya Yakobo na Yose, na pia mama ya wana wa Zebedayo.^j

57 Sasa kwa kuwa ilikuwa jioni, akaja tajiri mmoja wa Arimathea, aitwaye Yosefu,

27:50 *Tnn., “akaitoa roho yake.” Au “akakata pumzi.” **27:52** *Au “makaburi ya ukumbusho.”

ambaye pia alikuwa mwanafunzi wa Yesu.^a **58** Mtu huyu alienda kwa Pilato akaomba apewe mwili wa Yesu.^b Naye Pilato akaamuru apewe.^c **59** Yosefu akauchukua mwili huo, akaufunga kwa kitani bora kilicho safi,^d **60** akaulaza katika kaburi lake jipya,^e alilokuwa amechimba katika mwamba. Kisha akaviringisha jiwe kubwa kwenye mwingilio wa lile kaburi,^f akaondoka. **61** Lakini Maria Magdalene na yule Maria mwingine wakabaki hapo, wakiwa wameketi mbele ya kaburi.^f

62 Siku iliyofuata, baada ya Matayarisho,^g wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakakusanyika mbele ya Pilato, **63** wakisema: “Bwana, tumekumbuka mjanja huyo alipokuwa hai alisema, ‘Nitafufuliwa baada ya siku tatu.’^h **64** Kwa hiyo, amuru kaburi lilindwe mpaka siku ya tatu, ili wanafunzi wake wasije wakamwiba’ na kuwaambia watu, ‘Alifufuliwa kutoka kwa wafu!’ Kisha udanganyifu huu wa mwisho utakuwa mbaya zaidi kuliko ule wa kwanza.” **65** Pilato akawaambia: “Mnaweza kuweka walinzi. Nendeni mkalilinde jinsi mnavyotaka.” **66** Basi wakaenda na kulilinda kaburi kwa kulitia jiwe muhuri na kuweka walinzi.

28 Baada ya Sabato, kuli-pokuwa kukipambazuka siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalene na yule Maria mwingine wakaenda kuli-tazama kaburi./

2 Na tazama! tetemeko kubwa la ardhi lilikuwa limeto-

27:60 *Au “kaburi lake jipya la ukumbusho.” #Au “kaburi la ukumbusho.”

SURA YA 27

a Mk 15:42, 43
Lu 23:50-53

b Kum 21:22, 23

c Mk 15:45-47
Yoh 19:38

d Yoh 19:40, 41

e Isa 53:9

f Lu 23:55

g Mk 15:42
Lu 23:54
Yoh 19:14

h Mt 12:40
Yoh 2:19

i Mt 28:12, 13

SURA YA 28

j Mk 16:1
Lu 24:1
Lu 24:10
Yoh 20:1

Safu ya 2

a Mk 16:4, 5
Lu 24:2, 4

b Mdo 1:10

c Mk 16:6

d Mt 16:21
Mt 17:22, 23
1Ko 15:3, 4

e Mt 26:32
Mt 28:16
Mk 14:28

f Mk 16:7

g Mk 16:8
Lu 24:9

h Mt 27:65

kea, kwa maana malaika wa Yehova* alikuwa ameshuka kutoka mbinguni akaja na kuliviringisha lile jiwe, naye alikuwa amelikalialia.^a **3** Alikuwa aking’aa kama radi, na mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji.^b **4** Ndiyo, wale walinzi wakatetemeka, wakawa kama wafu kwa sababu ya kumwogopa.

5 Lakini malaika akawaambia wale wanawake: “Msio-gope, kwa maana ninajua mnamtafuta Yesu aliyeuawa kwenye mti.^c **6** Hayupo hapa, kwa maana amefufuliwa kama alivyosema.^d Njoo-ni, tazameni mahali alipokuwa amelala. **7** Basi nendeni upesi mkawaambie wanafunzi wake kwamba alifufuliwa kutoka kwa wafu, na tazama! anawatangulia kwenda Galilaya.^e Mtamwona huko. Tazama! Nimewaambia ninyi.”^f

8 Basi, wakaondoka upesi kwenye kaburi la ukumbusho wakiwa na hofu na shangwe kubwa. Wakakimbia kwenda kuwajulisha wanafunzi wake.^g **9** Na tazama! Yesu akakutana nao na kuwaambia: “Siku njema!” Wakamkaribia, wakamshika miguu na kumsujudia.* **10** Ndipo Yesu akawaambia: “Msio-gope! Nendeni, mkawajulisha ndugu zangu ili waende Galilaya, na huko wataniona.”

11 Walipoondoka na kwennda, baadhi ya walinzi^h wakaenda jijini na kuwajulisha wakuu wa makuhani mambo yote yaliyotokea. **12** Baada ya wakuu wa makuhani na wazee kukutana na kushauriana,

28:2 *Angalia Nyongeza A5. 28:9 *Au “kumwinamia.”

wakawapa wale wanajeshi kiasi kikubwa cha fedha **13** wakawaambia: “Semeni, ‘Wanafunzi wake walikuja usiku wakamwiba tulipokuwa tumelala usingizi.’^a **14** Na gavana akisikia, sisi tutamwelezea jambo hilo,* nanyi hamtahitaji kuwa na wasiwasi.” **15** Basi wakachukua zile fedha na kufanya kama walivyoagizwa, na hadithi hiyo imeenea miongoni mwa Wayahudi mpaka leo hii.

16 Hata hivyo, wale wanafunzi 11 wakaenda Galilaya^b kwenye mlima ambao

28:14 *Tnn., “tutamshawishi.”

SURA YA 28

a Mt 27:64

b Mt 26:32

Safu ya 2

a Iko 15:6

b Efe 1:20, 21
Flp 2:9

c Mdo 1:8
Ro 10:18
Ro 11:13
Ufu 14:6

d Mdo 2:38
Mdo 8:12

e Mdo 20:20
Iko 11:23
ZPe 3:1, 2
1Yo 3:23

f Mt 13:39
Mt 13:49
Mt 24:3

Yesu alikuwa amepanga kukutana nao.^a **17** Walipomwona wakasujudu,* lakini baadhii yao walikuwa na shaka. **18** Yesu akakaribia na kuwaambia: “Nimepewa mamlaaka yote mbinguni na duniani.^b **19** Basi, nendeni mkafanye wanafunzi kutoka kwa watu wa mataifa yote,^c mkiwabatiza^d katika jina la Baba na la Mwana na la roho takatifu, **20** na kuwafundisha kushika mambo yote niliyowaamuru.^e Na tazama! mimi nipo pamoja nanyi sikuzote mpaka umalizio wa mfumo wa mambo.”^{*f}

28:17 *Au “wakamwinamia.” **28:20** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

KULINGANA NA

MARKO

YALIYOMO

- Yohana Mbatizaji ahubiri (1-8)
Yesu abatizwa (9-11)
Shetani amjaribu Yesu (12, 13)
Yesu aanza kuhubiri huko Galilaya (14, 15)
Wanafunzi wa kwanza wachaguliwa (16-20)
Roho mwovu afukuzwa (21-28)
Yesu awaponya watu wengi huko Kapernaumu (29-34)
Yesu asali faraghani (35-39)
Mtu mwenye ukoma aponywa (40-45)
- Yesu amponya mtu aliyepooza (1-12)
Yesu amwita Lawi (13-17)
Swali kuhusu kufunga (18-22)
Yesu, ‘Bwana wa Sabato’ (23-28)
- Mwanamume mwenye mkono uliopooza aponywa (1-6)

- Umati mkubwa kando ya bahari (7-12)
Mitume 12 (13-19)
Kukufuru roho takatifu (20-30)
Mama na ndugu za Yesu (31-35)
- MIFANO KUHUSU UFALME (1-34)
Mpandaji (1-9)
Kwa nini Yesu alitumia mifano? (10-12)
Mfano wa mpandaji wafanuliwa (13-20)
Taa haiwekwi chini ya kikapu (21-23)
Kipimo unachopima (24, 25)
Mpandaji anayelala (26-29)
Mbegu ya haradali (30-32)
Kutumia mifano (33, 34)
Yesu atuliza dhoruba (35-41)
 - Yesu awaruhusu roho waovu waingie ndani ya nguruwe (1-20)

- Binti ya Yairo; mwanamke agusa vazi la nje la Yesu (21-43)
- 6 Yesu akataliwa katika mji wa nyumbani kwao (1-6)
Wale 12 wapewa maagizo kuhusu huduma (7-13)
Kifo cha Yohana Mbatizaji (14-29)
Yesu alisha wanaume 5,000 (30-44)
Yesu atembea juu ya maji (45-52)
Yesu awaponya watu huko Genesareti (53-56)
- 7 Yesu afunua mapokeo ya wanadamu (1-13)
Mtu huchafuliwa na kile kinachotoka moyoni (14-23)
Imani ya mwanamke wa Sirofoinike (24-30)
Mwanamume aliyekuwa kiziwi aponywa (31-37)
- 8 Yesu alisha wanaume 4,000 (1-9)
Waomba ishara (10-13)
Chachu ya Mafarisayo na ya Herode (14-21)
Mwanamume kipofu aponywa huko Bethsaida (22-26)
Petro amtambulisha Kristo (27-30)
Kifo cha Yesu chatabiriwa (31-33)
Wanafunzi wa kweli (34-38)
- 9 Yesu ageuka sura (1-13)
Mvulana aliyekuwa na roho mwovu aponywa (14-29)
Mambo yote yanawezekana kwa mtu mwenye imani (23)
Kifo cha Yesu chatabiriwa tena (30-32)
Wanafunzi wabishana kuhusu aliye mkuu zaidi (33-37)
Mtu asiyetupinga yuko upande wetu (38-41)
Vikwazo (42-48)
“Iweni na chumvi ndani yenu” (49, 50)
- 10 Ndoa na talaka (1-12)
Yesu awabariki watoto (13-16)
Swali la mwanamume tajiri (17-25)
Kujidhabihu kwa ajili ya Ufalme (26-31)
Kifo cha Yesu chatabiriwa tena (32-34)
Ombi la Yakobo na Yohana (35-45)
Yesu fidia kwa ajili ya wengi (45)
Bartimayo aliyekuwa kipofu aponywa (46-52)
- 11 Yesu aingia kwa kishindo (1-11)
Mtini walaaniwa (12-14)
Yesu asafisha hekalu (15-18)
Somo kutoka kwa mtini ulionyauka (19-26)
Wataka kujua chanzo cha mamlaka ya Yesu (27-33)
- 12 Mfano wa wakulima wauaji (1-12)
Mungu na Kaisari (13-17)
Swali kuhusu ufufuo (18-27)
Amri mbili kuu zaidi (28-34)
Je, Kristo ni mwana wa Daudi? (35-37a)
Waonywa wajihadhari na waandishi (37b-40)
Sarafu mbili za mjane maskini (41-44)
- 13 UMALIZIO WA MFUMO WA MAMBO (1-37)
Vita, matetemeko ya ardhi, njaa (8)
Habari njema itahubiriwa (10)
Dhiki kuu (19)
Kuja kwa Mwana wa binadamu (26)
Mfano wa mtini (28-31)
Endeleeni kukesha (32-37)
- 14 Makuhani wapanga njama ya kumuua Yesu (1, 2)
Yesu amiminiwa mafuta yenye marashi (3-9)
Yuda amsaliti Yesu (10, 11)
Pasaka ya mwisho (12-21)
Mlo wa Jioni wa Bwana waanzishwa (22-26)
Yesu atabiri kwamba Petro atamkana (27-31)
Yesu asali akiwa Gethsemane (32-42)
Yesu akamatwa (43-52)
Kesi mbele ya Sanhedrini (53-65)
Petro amkana Yesu (66-72)
- 15 Yesu mbele ya Pilato (1-15)
Adhihakwa hadharani (16-20)
Atundikwa kwenye mti huko Golgotha (21-32)
Yesu afa (33-41)
Yesu azikwa (42-47)
- 16 Yesu afufuliwa (1-8)

mbua, wewe Yesu Mnazareti?^a Je, umekuja kutuamamiza? Ninajua wewe ni nani, Mta-katifu wa Mungu!”^b **25** Laki-ni Yesu akamkemea, akise-ma: “Nyamaza, na umto-ke!” **26** Na yule roho mwovu, baada ya kumfanya mtu huyo agaegae na kupiga kelele kwa sauti kubwa, akamtoka. **27** Basi, watu wote wakasha-ngaa sana na kuulizana: “Ni jambo gani hili? Ni fundisho ji-pya! Hata anawaamuru roho waovu kwa mamlaka, nao wa-namtii!” **28** Basi habari ku-mhusu zikaenea upesi kila ma-hali katika eneo lote la Galilaya.

29 Ndipo wakatoka kwenye sinagogi na kwenda nyumba-ni kwa Simoni na Andrea wa-kiwa na Yakobo na Yohana.^c **30** Sasa mama mkwe wa Si-moni^d alikuwa amelala akiu-gua homa, na mara moja wa-kamwambia Yesu kumhusu. **31** Yesu akamkaribia, aka-mshika mkono na kumwinua. Akapona homa, naye akaanza kuwahudumia.

32 Ilipofika jioni, jua lilipo-tua, watu wakaanza kumletea wote waliokuwa wagonjwa na waliokuwa na roho waovu;^e **33** na jiji lote lilikuwa limeku-sanyika mlangoni. **34** Basi akawaponya watu wengi wa-liokuwa na magonjwa mbali-mbali,^f akafukuza roho wengi waovu, lakini hakuwaruhusu hao roho waovu waseme, kwa maana walijua yeye ni Kristo.*

35 Asubuhi na mapema, ku-lipokuwa bado na giza, akaa-mka na kutoka nje, akaenda mahali pasipo na watu, naye akaanza kusali.^g **36** Hata hi-

1:34 *Au labda, “walijua yeye ni nani.”

SURA YA 1

a Mt 8:28, 29

b Yak 2:19

c Mt 8:14, 15
Lu 4:38, 39

d Iko 9:5

e Mt 8:16
Lu 4:40, 41

f Isa 53:4

g Mt 14:23
Mk 14:32
Lu 4:42
Ebr 5:7

Safu ya 2

a Isa 61:1
Lu 4:43
Yoh 17:4

b Mt 4:23

c Mt 8:1, 2
Lu 5:12d Mt 8:3
Lu 5:13e Law 14:3, 4
Law 14:10, 11
Kum 24:8f Mt 8:4
Lu 5:14

g Lu 5:15

SURA YA 2

h Mt 4:13
Mt 9:1i Isa 61:1
Efe 2:17
Ebr 2:3

vyo, Simoni na wenzake wa-kamtafuta sana, **37** na wali-pompata wakamwambia: “Kila mtu anakutafuta.” **38** Lakini akawaambia: “Twendeni ma-hali pengine, katika miji iliyo karibu, ili nihubiri huko pia, kwa maana nilikuja kwa ku-sudi hilo.”^a **39** Naye akaenda akihubiri katika masinagogi yao katika Galilaya yote na ku-wafukuza roho waovu.^b

40 Mtu fulani mwenye uko-ma akamjia, akapiga magoti na kumwomba: “Ikiwa tu una-taka, unaweza kunitakasa.”^c

41 Ndipo akamsikitikia, aka-nyoosha mkono wake, aka-mgusa na kumwambia: “Ni-nataka! Takasika.”^d **42** Mara moja ule ukoma ukaisha, akawa safi. **43** Kisha aka-mpa maagizo thabiti na mara moja akamwacha aende, **44** akamwambia: “Usimwa-mbie jambo lolote mtu yeyote, bali nenda ukajionyeshe kwa kuhani na utoe vitu alivyoa-giza Musa kwa ajili ya kuta-kaswa kwako,^e ili kuwa usha-hidi kwao.”^f **45** Hata hivyo, baada ya kuondoka, mtu huyo akaanza kueneza habari hizo kila mahali, hivi kwamba Yesu hakuweza kuingia katika jiji lolote waziwazi, bali alikaa nje mahali pasipo na watu. Laki-ni watu walizidi kumjia kuto-ka kila upande.^g

2 Hata hivyo, baada ya siku kadhaa Yesu akarudi tena Kapernaumu na watu wakasi-kia kwamba yuko nyumba-ni.^h **2** Basi watu wengi sana wakaja hivi kwamba hapaku-wa na nafasi tena, hata mlan-goni, naye akaanza kuwahu-biria.ⁱ **3** Wakamletea mtu ali-yepooza, akiwa amebewa na

watu wanne.^a **4** Lakini kwa sababu ya umati, hawakuweza kumleta moja kwa moja kwa Yesu, basi baada ya kutoboa sehemu ya paa lililokuwa juu ya Yesu, wakamteremsha yule mtu aliyepooza, akiwa amelala juu ya kitanda.* **5** Yesu alipoona imani yao,^b akamwambia yule mtu aliyepooza: “Mwanangu, umesamehewa dhambi zako.”^c **6** Sasa baadhi ya waandishi waliolewa wameketi hapo wakaaanza kuwaza mioyoni mwao:^d **7** “Kwa nini mtu huyu anasema hivyo? Anakufuru. Ni nani anayeweza kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake?”^e **8** Lakini mara moja Yesu akatambua rohoni mwake kwamba walikuwa wakiwaza hivyo, basi akawaambia: “Kwa nini mnawaza mambo hayo katika mioyo yenu?” **9** Ni jambo gani rahisi zaidi, kumwambia mtu huyu aliyepooza, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema, ‘Simama, uchukue kitanda chako utembe?’ **10** Lakini ili mjue kwamba Mwana wa binadamu^g ana mamlaka ya kusamehe dhambi duniani—^h akamwambia yule mtu aliyepooza: **11** “Ninakuambia, Simama, chukua kitanda chako, uende nyumbani.” **12** Ndipo akasimama, na mara moja akachukua kitanda chake akatembea mbele yao wote na kwenda nje. Basi, wote wakashangaa, na kumtukuzwa Mungu wakisema: “Hatujawahi kamwe kuona jambo kama hilo.”ⁱ

13 Akaenda tena kando ya bahari; na umati uka-

2:4 *Au “machela.”

SURA YA 2

a Lu 5:18, 19

b Mdo 14:9, 10

c Isa 53:11
Mt 9:2
Lu 5:20
Lu 7:47, 48

d Mt 9:3-8
Lu 5:21-26

e Isa 43:25

f Mt 9:4
Lu 6:8
Ufu 2:23

g Da 7:13

h Isa 53:11

i Mt 9:33
Yoh 7:31
Yoh 9:32

Safu ya 2

a Mt 9:9
Lu 5:27, 28

b Mt 9:10, 11
Lu 5:29, 30

c Isa 61:1
Mt 9:12, 13
Lu 5:31, 32
Lu 19:10
1Ti 1:15

d Mt 9:14, 15
Lu 5:33-35

e Mt 22:2
2Ko 11:2
Ufu 19:7

f Lu 17:22

mjia, naye akaanza kuwafu-ndisha. **14** Alipokuwa aki-pita, akamwona Lawi mwana wa Alfayo akiwa ameketi kwenye ofisi ya kodi, akamwambia: “Njoo uwe mfuasi wangu.” Mara moja akasimama na kumfuata.^a **15** Baadaye alipokuwa akila* katika nyumba ya Lawi, wakusanya kodi wengi na watenda dhambi walikuwa wakila# pamoja na Yesu na wanafunzi wake, kwa maana wengi wao walikuwa wakimfuata.^b **16** Lakini waandishi wa Mafarisayo, walipoona akila na watenda dhambi na wakusanya kodi, wakaaanza kuwauliza wanafunzi wake: “Je, yeye hula pamoja na wakusanya kodi na watenda dhambi?” **17** Aliposikia hilo, Yesu akawaambia: “Watu wenye nguvu hawahitaji daktari, lakini wagonjwa wanahitaji. Sikuja kuwaita waadilifu, bali watenda dhambi.”^c

18 Wanafunzi wa Yohana na Mafarisayo walikuwa na zoea la kufunga. Basi wakaja na kumuuliza Yesu: “Kwa nini wanafunzi wa Yohana na wanafunzi wa Mafarisayo hufunga, lakini wanafunzi wako hawafungi?”^d **19** Yesu akawajibu: “Rafiki za bwana harusi^e hawahitaji kufunga wanapokuwa naye, sivyo? Bwana harusi akiwa pamoja nao hawawezi kufunga. **20** Lakini siku zitakuja ambapo bwana harusi ataondolewa kwao,^f ndipo watakapofunga siku hiyo. **21** Hakuna mtu anayeshona kiraka cha kitambaa kipya juu ya vazi la nje la zamani. Aki-fanya hivyo, kitambaa kipya

2:15 *Au “alipokuwa ameketi mezani.”
#Au “walikuwa wameketi mezani.”

kitatoka kwenye vazi la zamani, nalo litararuka vibaya zaidi.^a **22** Pia, hakuna mtu anayeweka divai mpya katika viriba vya divai vilivyochakaa. Akifanya hivyo, divai itapasua ngozi ya viriba naye atapoteza divai pamoja na ngozi. Lakini divai mpya huwekwa katika viriba vipya vya divai.”

23 Alipokuwa akipita kwenye mashamba ya nafaka siku ya Sabato, wanafunzi wake wakaanza kukata masuke ya nafaka huku wakitembea.^b

24 Hivyo, Mafarisayo wakamwambia: “Tazama sasa! Kwa nini wanafanya jambo lisi-lo halali siku ya Sabato?”

25 Lakini akawaambia: “Je, hamjasoma alilofanya Daudi, wakati alipokuwa na uhitaji na yeye na wanaume waliokuwa pamoja naye walipohisinja?^c **26** Jinsi katika simulizi kuhusu mkuu wa makuhanani Abiathari,^d Daudi alivyoi- ngia katika nyumba ya Mungu na kula mikate ya toleo,* ambayo si halali kwa mtu yeyote kula isipokuwa makuhanani,^e naye akawapa pia watu waliokuwa pamoja naye?”

27 Kisha akawaambia: “Sabato iliwekwa kwa ajili ya mwanadamu,^f bali si mwanadamu kwa ajili ya Sabato. **28** Basi, Mwana wa binadamu pia ndiye Bwana wa Sabato.”^g

3 Yesu akaingia tena ndani ya sinagogi, na palikuwa na mtu aliyepooza mkono.^h **2** Basi walikuwa wakimwanga- lia sana waone kama atamponya mtu huyo siku ya Sabato, ili wamshtaki. **3** Akamwambia yule mtu aliyepoo-

2:26 *Au “mikate iliyowekwa mbele za Mungu.”

SURA YA 2

a Mt 9:16, 17
Lu 5:36-38

b Mt 12:1-8
Lu 6:1-5

c 1Sa 21:1-6

d 1Sa 22:20

e Kut 25:30
Law 24:5-9

f Kut 20:9, 10

g Mt 12:8
Lu 6:5

SURA YA 3

h Mt 12:9-14
Lu 6:6-11

Safu ya 2

a Lu 14:1-3

b Yoh 12:39, 40

c Mt 22:16
Mk 12:13

d Mt 12:15

e Mt 9:20, 21
Mk 5:27, 28
Mk 6:56

f Mt 8:31

g Mk 1:23, 24
Mk 5:7
Lu 4:41

h Mt 12:15, 16
Mk 1:25

i Yoh 15:16

j Lu 6:12, 13

za mkono: “Simama uje hapa katikati.” **4** Kisha akawauliza: “Je, ni halali kufanya mema au kufanya mabaya siku ya Sabato, kuokoa uhai* au kuua?”^a Lakini wakanyamaza. **5** Akawatazama kwa hasira na kuhuzunika sana kwa sababu mioyo yao ilikuwa migumu,^b akamwambia mtu huyo: “Nyoosha mkono wako.” Akaunyoosha mkono wake, nao ukapona. **6** Ndipo Mafarisayo wakaenda nje na mara moja wakafanya mkutano pamoja na wafuasi wa chama cha Herode^c ili wamuee Yesu.

7 Lakini Yesu na wanafunzi wake wakaelekea baharini, na umati mkubwa kutoka Galilaya na Yudea ukamfuata.^d **8** Hata kutoka Yerusalemu, Idumea, ng'ambo ya Yordani, na maeneo ya Tiro na Sidoni, umati mkubwa ukamjia uliposikia kuhusu mambo mengi aliyokuwa akifanya. **9** Naye akawaambia wanafunzi wake wamletee mashua ndogo ili umati usimsonge. **10** Kwa sababu aliwaponya watu wengi, wote waliokuwa wagonjwa sana walikuwa wakimkaribia ili wamguse.^e **11** Hata roho waovu,^f kila mara walipomwona, walianguka mbele yake na kupaza sauti wakisema: “Wewe ndiye Mwana wa Mungu.”^g **12** Lakini mara nyingi aliwaagiza kwa kusisitiza wasimtangaze.^h

13 Akapanda mlimani na kuwaita wale aliwataka,ⁱ nao wakaja.^j **14** Akaanzisha* kikundi cha wanaume 12, ambao pia aliwaita mitume, nao wangepuatana naye, na

3:4 *Au “nafsi.” 3:14 *Au “Aka- chagua.”

angewatuma kuhubiri **15** na wangukuwa na mamlaka ya kufukuza roho waovu.^a

16 Kile kikundi cha wanau-me **12^b** alichozanza* kilikuwa na Simoni, ambaye pia ali-mwita Petro,^c **17** Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo (ambao pia aliwaita Boanerge, jina linalomaanisha “Wana wa Ngurumo”),^d **18** Andrea, Filipo, Bartholomayo, Mathayo, Tomasi, Yakobo mwana wa Alfayo, Thadayo, Simoni Mkananayo,* **19** na Yuda Iskariote, ambaye baadaye alimsaliti.

Kisha Yesu akaingia ndani ya nyumba, **20** na umati ukakusanyika tena, hivi kwamba hata hawakupata nafasi ya kula. **21** Lakini watu wake wa ukoo waliposikia hilo, wakaenda kumkamata, kwa maana walikuwa wakisema: “Amerukwa na akili.”^e **22** Pia, waandishi walio-shuka kutoka Yerusalemu walikuwa wakisema: “Ana Beelzebuli,* naye anawafukuza roho waovu kwa nguvu za mtawala wa roho waovu.”^f **23** Kisha akawaita na kuzungumza nao kwa mifano: “Shetani anawezaje kumfukuza Shetani? **24** Ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe, hawezi kusimama;^g **25** na nyumba ikigawanyika dhidi yake wenyewe, haiwezi kusimama. **26** Pia, ikiwa Shetani anajipinga mwenyewe na amegawanyika, hawezi kusimama, bali ataangamia. **27** Kwa kweli, hakuna yeyote anayeweza kuingia ndani ya nyumba ya mtu

3:16 *Au “alichochagua.” 3:18 *Au “mwenye bidii.” 3:22 *Jina lingine la Shetani.

SURA YA 3

a Mt 10:1

b Mt 10:2-4
Lu 6:14-16
Mdo 1:13

c Yoh 1:42

d Lu 9:54

e Yoh 7:5

f Mt 9:34
Mt 10:25
Mt 12:24-29
Lu 11:15
Yoh 8:48

g Lu 11:17,18

Safu ya 2

a Mt 12:31, 32
Lu 12:10b Ebr 6:4, 6
Ebr 10:26c Yoh 7:20
Yoh 10:20d Mt 13:55
Yoh 2:12
Mdo 1:14e Mt 12:46-50
Lu 8:19-21

f Mk 6:3

g Mt 12:49
Ebr 2:11h Mt 12:50
Lu 8:21
Yoh 15:14

SURA YA 4

i Mt 13:1, 2
Lu 8:4

j Mt 13:34

k Mt 13:3-9
Lu 8:5-8

l Mk 4:14

mwenye nguvu na kuiba mali zake isipokuwa kwanza amfungu mtu huyo. Hapo ndipo atakapoweza kuipora nyumba yake. **28** Kwa kweli nina-waambia kwamba wanadamu watasamehewa mambo yote, hata ziwe dhambi gani au maneno ya kukufuru wanayosema. **29** Lakini yeyote anayekufuru roho takatifu hatasamehewa milele,^a bali atakuwa na hatia ya dhambi ya milele.”^b **30** Alisema hivyo kwa sababu walikuwa wakisema: “Ana roho mwovu.”^c

31 Mama yake na ndugu zake^d wakaja na kusimama nje, wakamtuma mtu akamwite.^e **32** Kwa kuwa umati ulikuwa umeketi kumzunguka, wakamwambia: “Tazama! Mama yako na ndugu zako wako nje wanakuita.”^f **33** Lakini akawauliza: “Mama yangu na ndugu zangu ni nani?” **34** Akawatazama watu walioketi kumzunguka, akasema: “Tazama, mama yangu na ndugu zangu!”^g **35** Yeyote anayefanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, dada yangu, na mama yangu.”^h

4 Yesu akaanza tena kufundisha kando ya bahari, na umati mkubwa sana ukakusanyika karibu naye. Basi akapanda ndani ya mashua na kuketi humo mbali kidogo na ufuo, lakini umati wote ulikuwa kando ya bahari, ufuoni.ⁱ **2** Naye akaanza kuwafundisha mambo mengi kwa mifano,^j na alipokuwa akifundisha akasema:^k **3** “Sikilizeni. Tazama! Mpandaji alienda kupanda mbegu.^l **4** Alipokuwa akipanda, mbegu fulani zikaanguka kando ya barabara, ndege wakaja na kuzila.

5 Nyingine zikaanguka kwenye miamba, mahali pasipo na udongo mwingi, na mara moja zikachipuka kwa sababu udongo haukuwa na kina.^a

6 Lakini jua lilipochomoza, ziliungua na kunyauka kwa sababu hazikuwa na mizizi.

7 Mbegu nyingine zikaanguka kwenye miiba, nayo miiba ikakua na kuzisonga, nazo hazikuzaa matunda.^b 8 Lakini nyingine zikaanguka kwenye udongo mzuri, nazo zikakua na kuongezeka, zikaanza kuzaa matunda, mara 30, 60, na 100 zaidi.^c 9 Kisha akaongezea kusema: "Yule aliye na masikio ya kusikiliza, na asikilize."^d

10 Alipokuwa peke yake, wale waliokuwa karibu naye pamoja na wale 12 wakaaanza kumuuliza kuhusu mifano hiyo.^e 11 Akawaambia: "Ninyi mmepewa siri takatifu^f ya Ufalme wa Mungu, lakini kwa wale walio nje mambo yote yako katika mifano,^g 12 ili, ingawa wanatazama, watazama lakini wasione, na ingawa wanasikia, wasikie lakini wasielewe; wala wasigeuke na kusamehewa."^h 13 Tena akawaambia: "Ikiwa hamwelewi mifano huo, basi mtaelewaje mifano mingine yote?"

14 "Mpandaji hupanda neno.ⁱ 15 Basi, hawa ndio wale walio kando ya barabara ambapo neno hupandwa; lakini mara tu wanapolisikia, Shetani huja/ na kuliondoa neno lililopandwa ndani yao.^k 16 Vivyo hivyo, hawa ndio wale waliopandwa kwenye miamba; mara tu wanapolisikia neno, wanalikubali kwa shangwe.^l 17 Hata hivyo, hawana mizizi ndani yao, bali

SURA YA 4

a Mk 4:16, 17

b Mk 4:18, 19

c Mk 4:20

d Met 1:5
Mt 11:15
Lu 8:8e Mt 13:10
Lu 8:9f Efe 1:9, 10
Kol 1:26, 27g Mt 13:11
Lu 8:10h Isa 6:9, 10
Mt 13:13, 14
Yoh 12:40
Mdo 28:26i Mt 13:18
Lu 8:11
1Pe 1:25

j 1Pe 5:8

k Mt 13:19
Lu 8:12l Mt 13:20, 21
Lu 8:13

Safu ya 2

a Mt 13:22
Lu 8:14b Mt 6:25
Mt 24:38, 39c Met 23:4, 5
Mk 10:23
Lu 18:24
1Ti 6:9
2Ti 4:10

d 1Yo 2:16

e Mt 13:23
Lu 8:15f Mt 5:15
Lu 8:16, 17
Lu 11:33g Mt 10:26
Lu 12:2h Met 1:5
Mt 11:15
Ufu 2:7i Lu 8:18
Yak 1:25

j Mt 25:23

k Mt 13:12
Lu 8:18
Lu 19:26

wanaendelea kwa muda fulani; kisha mara tu wanapopata taabu au mateso kwa sababu ya lile neno, wanakwazika. 18 Bado kuna wengine ambao wamepandwa kwenye miiba. Hawa ndio wale wanaolisikia neno,^a 19 lakini mahangaiko^b ya mfumo huu wa mambo* na nguvu za udanganyifu za utajiri^c na tamaa^d za mambo mengine yote huingia na kulisonga neno, nalo halizai matunda.

20 Mwishowe, wale waliopandwa kwenye udongo mzuri ni wale wanaolisikiliza neno na kulipokea vizuri na kuzaa matunda—mara 30, 60, au 100 zaidi.^e

21 Akaendelea kuwaambia: "Je, taa huletwa na kuwekwa chini ya kikapu* au chini ya kitanda? Je, hailetwi na kuwekwa juu ya kinara cha taa?^f 22 Kwa maana hakuna jambo lolote lililofichwa ambalo halitafichuliwa; hakuna jambo lolote lililofunikwa kwa uangalifu ambalo halitafunuliwa.^g 23 Yeyote aliye na masikio ya kusikiliza, na asikilize."^h

24 Tena akawaambia: "Sikilizeni kwa makini mambo mnayosikia.ⁱ Kwa kipimo mnachopima, ndicho mtakachopimiwa, ndiyo, mtaongeze wa hata zaidi. 25 Kwa maana aliye na kitu ataongezewa,^j lakini yule asiye na kitu, hata kile alichu nacho kitachukuliwa."^k

26 Basi akaendelea kusema: "Kwa hiyo Ufalme wa Mungu ni kama vile mtu anapandama mbegu kwenye udongo. 27 Yeye hulala

4:19 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo." 4:21 *Au "kikapu cha kupimia."

usiku na kuamka mchana, nazo mbegu huota na kuwa ndefu—naye hajui jinsi zinaavyokua. **28** Udongo wenye-we hutokeza mazao hatua kwa hatua, kwanza jani, kisha suke, mwishowe nafaka iliyo-komaa ndani ya suke. **29** Lakini mimea inapokuwa tayari, yeye hutumia mundu, kwa sababu wakati wa kuvuna ume-fika.”

30 Akaendelea kusema: “Tutafanisha Ufalme wa Mungu na nini, au tutatumia mfano gani kuufafanua? **31** Ni kama mbegu ya haradali, ambayo ilipopandwa katika udongo ilikuwa ndogo kuliko mbegu zote duniani.^a **32** Lakini baada ya kupandwa, humea na kuwa kubwa kuliko mboga nyingine zote na kutokeza matawi makubwa, hivi kwamba ndege wa angani hupata makao chini ya kivuli chake.”

33 Akitumia mifano^b mingi kama hiyo, aliwafundisha neno kwa kadiri walivyoweza kusikiliza. **34** Kwa kweli, hakuwa akizungumza nao bila mfano, lakini alipokuwa na wanafunzi wake faraghani aliwafafanulia mambo yote.^c

35 Ilipofika jioni siku hiyo, akawaambia wanafunzi wake: “Tuvuke twende ng’ambo ya bahari.”^d **36** Baada ya kuuga umati, wakaenda pamoja na Yesu katika mashua, kama alivyokuwa, na kuli-kuwa na mashua nyinginezo pamoja naye.^e **37** Dhoruba kali ya upepo ikaanza kuvuma, mawimbi yakaipiga mashua, hivi kwamba ikakaribia kuzama.^f **38** Lakini Yesu alikuwa kwenye tezi, akiwa ame-

SURA YA 4

a Mt 13:31, 32
Lu 13:18, 19

b Zb 78:2

c Mt 13:11
Mt 13:34, 35
Mk 4:11

d Mt 8:18

e Mt 8:23
Lu 8:22

f Mt 8:24-27
Lu 8:23-25

Safu ya 2

a Zb 89:9

b Yoh 6:19

SURA YA 5

c Mt 8:28
Lu 8:26, 27

d Lu 8:28-30

e Mt 8:29
Yak 2:19

f Mdo 16:17, 18

lalia mto. Basi wakamwamsha na kumwambia: “Mwalimu, je, hujali kwamba tunakaribia kuangamia?” **39** Ndipo akasimama, akaukemea upepo na kuiambia bahari: “Nyamaza! Tulia!”^a Upepo ukakoma, kukawa shwari kabisa. **40** Basi akawauliza: “Kwa nini mnaogopa sana?”* Je, bado hamna imani?” **41** Lakini wakaogopa sana, nao wakaulizana: “Kwa kweli, mtu huyu ni nani, hivi kwamba upepo na bahari vinamtii?”^b

5 Basi, wakafika ng’ambo ya bahari na kuingia katika eneo la Wagerasene.^c **2** Mara tu Yesu alipotoka kwenye mashua akakutana na mtu mwenye roho mwovu akitoka makaburini.* **3** Alikuwa akikaa makaburini, na kufikia wakati huo hakuna mtu yeyote aliyeweza kumfunga kabisa hata kwa mnyororo. **4** Alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo, lakini aliikata minyororo na kuzivunja pingu; na hakuna mtu aliyeweza kumzuia. **5** Siku zote, usiku na mchana alikuwa akipaza sauti makaburini na milimani na kujikatakata kwa mawe. **6** Lakini alipomwona Yesu kwa mbali, alimkimbilia na kumwinamia.^d **7** Kisha akapaza sauti na kusema: “Kwa nini unanisumbua, Yesu, Mwana wa Mungu Aliye Juu Zaidi? Ninakuapisha kwa Mungu usinitese.”^e **8** Kwa maana Yesu alikuwa akimwambia: “Mtoke mtu huyu, wewe roho mwovu.”^f **9** Lakini Yesu akamuu-liza: “Unaitwa nani?” Naye

4:40 *Au “kwa nini mna hofu?” 5:2

*Au “makaburi ya ukumbusho.”

akamwambia: “Jina langu ni Kikosi, kwa sababu tuko wengi.” **10** Naye akamsihi sana Yesu asiwafukuze roho hao kutoka katika nchi hiyo.^a

11 Sasa kulikuwa na nguruwe wengi^b wakila hapo mlimani.^c **12** Basi hao roho waovu wakamsihi: “Turuhusu tuingie ndani ya wale nguruwe.”

13 Naye akawaruhusu. Ndi-po wale roho waovu wakato-ka na kuingia ndani ya wale nguruwe, kisha lile kundi likatimua mbio, likaruka poromoko* na kuzama baharini. Wali-kuwa karibu 2,000, nao waka-fa maji baharini. **14** Lakini wachungaji wa nguruwe hao wakakimbia wakapeleka habari jijini na mashambani, watu wakaja kuona kilichotukia.^d

15 Basi wakamjia Yesu, wakamwona yule mtu aliyeku-wa na roho waovu, ambaye mwanzoni alikuwa na kile ki-kosi, akiwa ameketi, amevaa nguo, na akiwa na akili tima-mu, nao wakaogopa. **16** Pia, wale walioona tukio hilo wa-kawasimulia mambo yaliyo-mpata mtu huyo aliyekuwa na roho waovu na kuhusu wale nguruwe. **17** Basi wakaanza kumsihi Yesu aondoke katika eneo lao.^e

18 Alipokuwa akipanda ma-shua, yule mtu aliyekuwa na roho waovu akaanza ku-msihi aende pamoja naye.^f

19 Hata hivyo, hakumruhu-su, bali alimwambia: “Nen-da nyumbani kwa watu wako wa ukoo, ukawaambie mambo yote ambayo Yehova* ameku-fanyia na jinsi alivyokuonye-sha rehema.” **20** Mtu huyo

5:13 *Au “ukingo wenye mteremko mka-li.” 5:19 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 5

a Lu 8:31

b Lu 11:7, 8
Kum 14:8

c Mt 8:30-33
Lu 8:32-34

d Lu 8:35-37

e Mt 8:34

f Lu 8:38, 39

Safu ya 2

a Lu 8:40

b Mt 9:18
Lu 8:41, 42

c Lu 4:40

d Lu 15:25

e Mt 9:20-22
Lu 8:43, 44

f Mt 14:36
Mk 6:56

g Mt 9:21

h Lu 5:17
Lu 6:19

akaenda zake akaanza ku-tangaza katika Dekapoli* mambo yote ambayo Yesu alimfanyia, na watu wote waka-shangaa.

21 Baada ya Yesu kuvuka tena ng'ambo ya bahari kwa mashua, umati mkubwa ukakusanyika karibu naye ali-pokuwa kando ya bahari.^a

22 Sasa mmoja wa maofisa wasimamizi wa sinagogi, ali-yeitwa Yairo akaja, na alipo-mwona Yesu, akaanguka mi-guuni pake.*^b **23** Akamsi-hi mara nyingi, akisema: “Bi-nti yangu mdogo ni mgonjwa sana.* Tafadhali njoo uweke mikono yako juu yake^c ili apo-ne na kuishi.” **24** Ndipo Yesu akaenda pamoja naye, na umati mkubwa ulikuwa uki-mfuata na kumsonga.

25 Sasa kuna mwanamke aliyekuwa na mtiririko wa damu^d kwa miaka 12.^e **26** Ali-kuwa ameteseka sana* mi-kononi mwa madaktari wen-gi na alikuwa ametumia mali yake yote, na hakuwa amepo-na, badala yake hali yake ili-zidi kuwa mbaya. **27** Aliposi-ka kumhusu Yesu, akapenya katika umati nyuma ya Yesu na kuligusa vazi lake la nje,^f **28** kwa maana alikuwa aki-sema: “Nikiyagusa tu ma-vazi yake ya nje, nitapona.”^g **29** Papo hapo mtiririko wake wa damu ukakoma, naye aka-hisi mwilini mwake kwamba alikuwa amepona ule ugonjwa mbaya.

30 Mara moja Yesu akahisi ndani yake kwamba nguvu^h

5:20 *Au “Eneo lenye Majiji Kumi.”

5:22 *Au “akapiga magoti mbele yake.”

5:23 *Au “anakaribia kufa.” 5:26 *Au “alikuwa ameumizwa sana.”

zimemtoka, akaugeukia umati na kuuliza: “Ni nani aliyegusa mavazi yangu ya nje?”^a

31 Lakini wanafunzi wake wakamwambia: “Unaona jinsi umati unavyokusonga, na unauliza, ‘Ni nani aliyenigusa?’” **32** Hata hivyo, alikuwa akitazama ili aone mtu aliyekuwa amefanya hivyo. **33** Yule mwanamke aki-
jua lililompata, akaja akitetemeka kwa hofu akaanguka chini mbele yake, akamwambia ukweli wote. **34** Yesu akamwambia: “Binti yangu, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani,^b umepona ugonjwa wako mbaya.”^c

35 Alipokuwa bado anazungumza, watu fulani kutoka nyumbani kwa yule ofisa msimamizi wa sinagogi wakaja na kusema: “Binti yako amekufa! Kwa nini uendelee kumsumbua Mwalimu?”^d **36** Lakini Yesu akasikia maneno yao naye akamwambia yule ofisa msimamizi wa sinagogi: “Usiogope, uwe tu na imani.”^e **37** Hakumruhusu mtu yeyote amfuata isipokuwa Petro, Yakobo, na Yohana ndugu ya Yakobo.^f

38 Wakafika kwenye nyumba ya yule ofisa msimamizi wa sinagogi, Yesu akaona mvurugo wa watu walio-
kuwa wakilia na kuomboleza kwa sauti kubwa.^g **39** Baada ya kuingia, akawaambia: “Kwa nini mnaomboleza na kuleta mvurugo? Mtoto hajafa bali amelala usingizi.”^h **40** Ndipo wakaanza kumcheka kwa dhara-
rau. Lakini baada ya kuwatoa wote nje, akamchukua baba na mama ya yule mto-

5:36 *Au “onyesha tu imani.”

SURA YA 5

a Lu 8:45-48

b Lu 7:50
Lu 8:48

c Mt 9:22

d Lu 8:49

e Lu 8:50
Yoh 11:39, 40

f Mt 17:1
Mt 26:36, 37

g Mt 9:23-26
Lu 8:51-56

h Lu 8:52
Yoh 11:11

Safu ya 2

a Mt 9:25
Lu 7:14
Lu 8:54
Mdo 9:40

b Mk 1:42-44
Mk 7:35, 36

SURA YA 6

c Lu 4:16

d Yoh 6:42
Yoh 7:15

e Mt 13:54-58

f Isa 53:2

g Yoh 6:42

h Gal 1:19

i Mk 3:31

j Mt 13:57
Lu 4:24
Yoh 4:44

to pamoja na wanafunzi wake, akaingia mahali alipokuwa huyo mtoto. **41** Kisha akaushika mkono wa msichana huyo na kumwambia: “*Tali-
tha kumi,*” maneno ambayo yanapotafsiriwa, yanamaanisha: “Msichana mdogo, nina-
kuambia, inuka!”^a **42** Mara moja yule msichana akasimama akaanza kutembea. (Alikuwa na umri wa miaka 12.) Ndipo wakawa na shangwe kubwa sana. **43** Lakini akawaagiza tena na tena* wasimwambie mtu yeyote kuhusu jambo hilo,^b naye akawaambia wampe mtoto huyo chakula.

6 Akaondoka huko na kwenenda kwenye eneo lake la nyumbani,^c na wanafunzi wake wakamfuata. **2** Ili-
pofika siku ya Sabato, akaanza kufundisha katika sinagogi, na wengi waliomsikiliza wakashangaa na kusema: “Mtu huyu alitoa wapi mambo haya?^d Kwa nini alipewa hekima hii, na kwa nini matendo haya yenye nguvu yafanywe kupitia mikono yake?^e **3** Je, huyu si yule seremala^f mwana wa Maria^g na ndugu ya Yakobo,^h Yosefu, Yuda, na Simoni?ⁱ Na dada zake wapo hapa pamoja nasi, sivyo?” Basi wakaanza kukwazika kwa saba-
ba yake. **4** Lakini Yesu akawaambia: “Nabii anaheshimiwa kila mahali isipokuwa katika eneo lake la nyumbani na kati ya watu wake wa ukoo, na katika nyumba yake mwenyewe.”^j **5** Basi, hakuweza kufanya matendo yoyote yenye nguvu huko isipokuwa kuweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache na ku-

5:43 *Au “akawaamuru kwa uthabiti.”

waponya. **6** Kwa kweli, alishangaa sana kwa sababu hawakuwa na imani. Naye akaenda akizunguka vijijini, akifu-disha.^a

7 Sasa akawaita wale 12 akaanza kuwatuma wawili wawili,^b naye akawapa mamlaka juu ya roho waovu.^c **8** Pia, akawaagiza wasibebe chochote kwa ajili ya safari isipokuwa fimbo—wasibebe mka-te, mfuko wa chakula, wala pesa* kwenye mishipi yao^d—**9** bali wavae viatu lakini wasivae mavazi mawili.* **10** Pia, akawaambia: “Mtakapoingia katika nyumba yoyote, kaeni humo mpaka mtakapoondoka huko.^e **11** Na mahali popote ambapo watu hawatawakaribisha wala kuwasikiliza, mnapoondoka kung’uteni mavumbi yaliyo kwenye miguu yenu ili kuwa ushahidi kwao.”^f **12** Basi wakaondoka na kuhubiri kwamba watu wanapaswa kutubu,^g **13** pia wakafukuza roho wengi waovu^h na kuwapaka mafuta wagonjwa wengi na kuwaponya.

14 Mfalme Herode akasikia habari hizo, kwa maana jina la Yesu lilijulikana sana na watu walikuwa wakisema: “Yohana Mbatizaji amefufuliwa kutoka kwa wafu, ndiyo sababu anafanya matendo yenye nguvu.”ⁱ **15** Lakini wengine walikuwa wakisema: “Ni Eliya.” Pia, wengine wakasema: “Ni nabii kama manabii wa kale.”^j **16** Lakini Herode alipopata habari hizo akasema: “Yule Yohana niliyemkata kichwa, amefufuliwa.” **17** Kwa maana Herode alikuwa ameagiza Yohana aka-

SURA YA 6

a Mt 9:35
Lu 13:22

b Lu 10:1

c Mt 10:1
Lu 9:1-6

d Mt 10:9,10

e Mt 10:11

f Mt 10:14
Lu 10:10,11
Mdo 13:50, 51

g Mdo 2:38
Mdo 3:19

h Lu 10:17

i Mt 14:1-5
Lu 9:7-9

j Mt 16:14
Mk 8:28

Safu ya 2

a Lu 3:19, 20

b Law 18:16
Law 20:21

c Mt 11:11
Mt 21:26

d Mwa 40:20-22

e Mt 14:6-12

f Mt 14:8

matwe na kufungwa gerezani kwa sababu ya Herodia, mke wa Filipo ndugu yake. Kwa sababu Herode alikuwa amemwoa.^a **18** Kwa maana Yohana alikuwa akimwambia Herode: “Si halali kwako kuwa na mke wa ndugu yako.”^b **19** Basi Herodia alikuwa na kinyongo kumwelekea Yohana na alitaka kumuua, lakini hakuweza. **20** Kwa maana Herode alimwogopa Yohana kwa kuwa alijua ni mtu mwadilifu na mtakatifu,^c naye alikuwa akimlinda. Baada ya kumsikiliza, hakujua la kufanya, lakini bado aliendelea kumsikiliza kwa furaha.

21 Nafasi ilipatikana Herode alipoandaa mlo wa jioni kwenye sherehe ya sikukuu yake ya kuzaliwa.^d Akawaalika maafisa wake wa cheo cha juu, makamanda wa jeshi, na watu mashuhuri zaidi wa Galilaya.^e **22** Binti ya Herodia akaingia, akacheza dansi na kumfurahisha Herode na wageni wake.* Mfalme akamwambia msichana huyo: “Niombe chochote unachotaka, nami nitakupa.” **23** Ndiyo, akamwambia: “Chochote utakachomba nitakupa, hata ikiwa ni nusu ya ufalme wangu.” **24** Akaondoka na kwenda kumuuliza mama yake: “Niombe nini?” Akamwambia: “Kichwa cha Yohana Mbatizaji.” **25** Akarudi haraka mbele ya mfalme na kutoa ombi lake, akisema: “Nataka unipe sasa hivi kwenye sinia kichwa cha Yohana Mbatizaji.”^f **26** Inga mfalme alihuzunika sana, hakutaka kupuuza ombi lake, kwa sababu ya viapo vyake na

6:8 *Tnn., “shaba.” 6:9 *Au “vazi la ziada.”

6:22 *Au “wale waliokuwa wameketi mezani.”

wageni wake.* **27** Mara moja mfalme akamtuma mlinzi na kumwamuru alete kichwa cha Yohana. Basi akaenda gereza ni na kumkata kichwa, **28** akakileta kwenye sahani. Akampa yule msichana, na huyo msichana akampa mama yake. **29** Wanafunzi wake waliposikia jambo hilo, wakaja na kuuchukua mwili wake wakaulaza kaburini.*

30 Mitume wakamzunguka Yesu na kumwambia mambo yote waliyokuwa wamefanya na kufundisha.^a **31** Naye akawaambia: "Twendeni faraghani mahali pasipo na watu ili mpumzike kidogo."^b Kwa maana wengi walikuwa wakija na kwenda, nao hawakuwa na wakati hata wa kula. **32** Basi wakapanda mashua na kwenda mahali pasipo na watu ili wawe peke yao.^c **33** Lakini watu wakawaona wakienda na wengi wakajua jambo hilo. Watu kutoka majiji yote wakakimbia kwa miguu wakafika huko mbele yao. **34** Basi, aliposhuka, akaona umati mkubwa, akawasikitikia,^d kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji.^e Naye akaanza kuwafundisha mambo mengi.^f

35 Ilipokaribia jioni wanafunzi wake wakaja na kumwambia: "Mahali hapa hapana watu, na muda umesonga sana.^g **36** Waambie wao ndoke, waende wakajinunulie chakula katika maeneo ya mashambani na vijiji vilivyo karibu."^h **37** Akawajibu: "Ninyi wapeni chakula." Nao waka-

6:26 *Au "wale waliokuwa wameketi mezani." 6:29 *Au "katika kaburi la ukumbusho."

SURA YA 6

a Lu 9:10

b Mt 11:29
Mt 14:13

c Yoh 6:1, 2

d Mt 14:14
Ebr 4:15e 1Fa 22:17
Isa 53:6
Eze 34:5, 8
Mt 9:36f Isa 61:1
Lu 9:11g Mt 14:15-21
Lu 9:12-17

h Yoh 6:5

Safu ya 2

a 2Fa 4:42-44
Mt 15:33
Yoh 6:7

b Yoh 6:9

c Yoh 6:10-13

d Mk 8:6
Lu 24:30
Mdo 27:35e Mt 14:20
Lu 9:17
Yoh 6:13

f Mt 14:22

g Mt 6:6
Mt 14:23
Mk 1:35
Lu 6:12h Mt 14:24-33
Yoh 6:16-21

mwambia: "Je, twende tukanunue mikate ya dinari* 200 na kuwapa watu wale?"^a

38 Akawaambia: "Mna mikate mingapi? Nendeni mkaangalie!" Baada ya kuhakikisha, wakasema: "Mikate mitano na samaki wawili."^b **39** Akawaagiza watu wote waketi katika vikundi kwenye nyasi.^c **40** Basi wakaketi katika vikundi vya watu 100 na vya watu 50. **41** Akachukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni akatoa baraka.^d Kisha akaimega mikate na kuanza kuwapa wanafunzi ili wawape watu, naye akawagawanya wale samaki wawili kwa ajili ya watu wote. **42** Basi wote wakala wakashiba, **43** nao wakakusanya vipande vilivyobaki na kujaza vikapu 12, bila kuhesabu samaki.^e **44** Wale walio-kula mikate hiyo walikuwa wanaume 5,000.

45 Kisha, bila kukawia, akawaagiza wanafunzi wake wapande mashua watangulie kuelekea Bethsaida ng'ambo ya bahari, huku yeye akiuaga umati.^f **46** Lakini baada ya kuwaaga, akaenda mlimani kusali.^g **47** Ilipofika jioni, mashua ilikuwa katikati ya bahari, lakini yeye alikuwa peke yake kwenye nchi kavu.^h **48** Alipowaona wanafunzi wake wakitaabika kupiga makasia kwa kuwa upepo ulikuwa ukivuma kinyume chao, usiku karibu kesho la nne* akawaenda akitembea juu ya bahari; lakini alitaka[#] kuwapita. **49** Walipomwona aki-

6:37 *Angalia Nyongeza B14. 6:48 *Yaani, karibu saa 9 usiku hadi karibu saa 12 asubuhi. #Au "alikuwa karibu."

tembea juu ya bahari waka-fikiri: “Ni mzuka!” Nao waka-paza sauti. **50** Kwa maana wote walimwona, wakahangai-ka. Lakini mara moja akawaambia: “Jipeni moyo! Ni mimi; msioCOPE.”^a **51** Kisha akapanda kwenye mashua, na upepo ukatulia. Nao wakashangaa sana, **52** kwa maana hawakuwa wamefahamu maana ya ule muujiza wa mikate, bado mioyo yao ilikuwa mizito isiweze kuelewa.

53 Walipovuka bahari, wakafika Genesareti na kutia nanga hapo karibu.^b **54** Lakini mara tu waliposhuka kutoka kwenye mashua, watu wakamtambua. **55** Wakakimbia katika eneo hilo lote na kuanza kuleta wagonjwa wakiwa kwenye vitanda* mahali waliposikia Yesu yuko. **56** Na kila mahali alipokwenda katika vijiji, majiji, au mashambani watu waliwaweka wagonjwa sokoni, na kumsihi waguse tu upindo wa vazi lake la nje.^c Na wote waliogusa wakapona.

7 Sasa Mafarisayo na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu wakakusanyika kumzunguka Yesu.^d **2** Wakaona baadhi ya wanafunzi wake wakila chakula kwa mikonono isiyu safi, yaani, bila kunawa.* **3** (Kwa maana kabla ya kula, Mafarisayo na Wayahudi wote hunawa mikonono yao mpaka kwenye kiwiko, kwa kuyashika mapokeo ya mababu zao, **4** na wanapotoka sokoni, hawali chakula kabla ya kujisafisha. Kuna mapokeo mengine mengi amba-

6:55 *Au “machela.” 7:2 *Yaani, haikuwa imesafishwa kisherehe.

SURA YA 6

a Mt 14:27
Yoh 6:20

b Mt 14:34-36

c Mt 9:20
Mk 5:25-28
Lu 8:43, 44
Mdo 19:11, 12

SURA YA 7

d Mt 15:1

Safu ya 2

a Mt 23:25
Lu 11:38, 39

b Mt 15:2

c Mt 15:7-9

d Isa 29:13

e Gal 1:14
Kol 2:8

f Mt 15:3-6

g Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:2

h Kut 21:17
Law 20:9
Met 20:20

i 1Ti 5:8

j Mt 15:6

k Mk 7:3

l Mt 15:10

yo wamepokea na kuyashika, kama vile kubatiza* vikombe, mitungi, na vyombo vya shaba.)^a **5** Basi Mafarisayo na waandishi hao wakamuuliza: “Kwa nini wanafunzi wako hawafuati mapokeo ya mababu zetu, bali wanakula kwa mikonono isiyu safi?”^b **6** Akawaambia: “Isaya kwa kufaa alitoa unabii kuwahusu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, ‘Watu hawa huniheshimu kwa midomo yao, lakini mioyo yao iko mbali nami.’^c **7** Wao huniabadu bure, kwa maana wanafundisha amri za wanadamu kuwa mafundisho.’^d **8** Mnaiacha amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu.”^e

9 Akaendelea kuwaambia: “Mnapuuzua amri ya Mungu kwa ujanja ili mfuata mapokeo yenu.^f **10** Kwa mfano, Musa alisema, ‘Mheshimu baba yako na mama yako,’^g na, ‘Yeyote anayemtukana* baba yake au mama yake anapaswa kuuawa.’^h **11** Lakini ninyi mnasema, ‘Mtui akimwambia baba yake au mama yake: “Chochote nilicho nacho ambacho kingekusaidia ni korbani, (yaani, zawadi iliyo-wekwa wakfu kwa Mungu),”ⁱ **12** hivyo mnamzuia kumsaidia kwa chochote baba yake au mama yake.^j **13** Kwa hiyo, mnalibatilisha neno la Mungu kwa mapokeo yenu ambayo mlipewa.^j Nanyi mnafanya mambo mengine mengi kama hayo.”^k **14** Basi Yesu akauita tena umati, akawaambia: “Nisikilizeni, ninyi nyote, na mwelewe maana yake.^l

7:4 *Au “kuzamisha.” 7:10 *Au “Anayesema vibaya kumhusu.”

15 Mtu hawezi kuchafuliwa na kitu kinachoingia ndani yake; bali huchafuliwa na mambo yanayotoka ndani yake.”^a **16** *—

17 Alipouacha umati, Yesu aliingia ndani ya nyumba, na wanafunzi wake wakaanza kumuuliza kuhusu mfano huo.^b

18 Basi akawaambia: “Je, ni nyi pia hamwelewi kama wao? Je, hamjui kwamba mtu hawezi kuchafuliwa na kitu kinachoingia ndani yake, **19** kwa kuwa hakiingii moyoni mwake bali huingia tumboni, kisha hutoka na kuingia chooni?” Kwa hiyo akatanga za vyakula vyote kuwa safi. **20** Tena akasema: “Kile kina-choitoka ndani ya mtu ndicho humchafua.”^c **21** Kwa maana kutoka ndani, moyoni mwa watu,^d hutoka mawazo mabaya: uasherati,* wizi, mauaji, **22** uzinzi, pupa, uovu, udanganyifu, mwenendo mpotovu,* jicho lenye wivu, makufuru, majivuno, na ukosefu wa akili. **23** Mambo hayo yote maovu hutoka ndani, nayo humchafua mtu.”

24 Akatoka huko na kwenenda kwenye maeneo ya Tiro na Sidoni.^e Akaingia katika nyumba na hakutaka mtu yeyote ajue, lakini hakuweza kuepuka kutambuliwa. **25** Mara moja mwanamke ambaye binti yake mdogo alikuwa na roho mwovu akasikia kumhusu Yesu, akaja na kuanguka miguuni pake.^f **26** Mwanamke huyo

7:16 *Angalia Nyongeza A3. 7:21 *Wingi wa neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 7:22 *Au “ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu.” Kigiriki, *a-sel/gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 7

a Mt 15:11
Tit 1:15

b Mt 15:15-20

c Mt 15:18

d Mwa 6:5
Mwa 8:21
Yer 17:9

e Mt 15:21

f Mt 15:22-28

Safu ya 2

a Mt 10:5, 6
Mt 15:26
Ro 9:4
Efe 2:12

b Mt 15:28

c Yoh 4:49-51

d Mt 15:29

e Mt 9:32, 33
Lu 11:14

f Mk 8:23
Yoh 9:6

g Isa 35:5
Mt 11:5
Mt 15:30

h Isa 42:2
Mt 8:3, 4
Mk 5:42, 43

i Mk 1:43-45

j Mdo 14:11

alikuwa Mgiriki, wa taifa la* Sirofoinike; naye aliendelea kumsihi sana Yesu amfukuze roho mwovu aliyekuwa ndani ya binti yake. **27** Lakini Yesu akamwambia: “Kwanza acha watoto washibe, kwa maana haifai kuchukua mkate wa watoto na kuwatupia mbwa wadogo.”^a **28** Hata hivyo, yule mwanamke akamjibu: “Ndiyo, bwana, lakini hao mbwa wadogo walio chini ya meza hula makombo ya watoto wadogo.” **29** Ndipo Yesu akamwambia: “Kwa sababu umesema hivyo, nenda; yule roho mwovu amemtoka binti yako.”^b **30** Basi akaenda nyumbani akamkuta yule mtoto akiwa amelala kitandani, na yule roho mwovu alikuwa amemtoka.^c

31 Yesu aliporudi kutoka eneo la Tiro akapitia Sidoni, Dekapoli,* na kufika Bahari ya Galilaya.^d **32** Basi wakamletea mtu aliye kiziwi na mwenye tatizo la kuzungumza,^e nao wakamsihi aweke mkono juu yake. **33** Kisha akampeleka faraghani, mbali na umati. Halafu akamtia vidole masikioni, baada ya kutema mate, akamgusa ulimi.^f **34** Yesu akatazama mbinguni, akavuta pumzi kwa nguvu na kumwambia: “*Efatha*,” yaani, “Funguka.” **35** Ndipo masikio yake yaka-funguliwa,^g na tatizo lake la kuzungumza likaisha, naye akaanza kuzungumza vizuri. **36** Kisha akawaamuru wasimwambie mtu yeyote,^h lakini kadiri alivyowakataza, ndivyo walivyozidi kutangaza jambo hilo.ⁱ **37** Kwa kweli, walishangaa sana^j wakasema: “Ame-

7:26 *Au “aliyezaliwa huko.” 7:31 *Au “Eneo lenye Majiji Kumi.”

fanya mambo yote vema. Hata anafanya viziwi wasikie na wasio na uwezo wa kusema, wazungumze.”^a

8 Siku hizo umati mkubwa ukakusanyika tena, na hawakuwa na chakula. Basi, akawaita wanafunzi na kuwaambia: **2** “Ninausikitikia umati,^b kwa sababu tayari wamekaa pamoja nami siku tatu nao hawana chakula.”^c **3** Ni kiwaacha waende nyumbani wakiwa na njaa,* watazimia njiani, na baadhi yao wametoka mbali.” **4** Lakini wanafunzi wake wakamjibu: “Tutapata wapi mikate ya kuwatoshwa watu hawa mahali hapa pasipo na watu?” **5** Ndipo akawauliza: “Mna mikate mingapi?” Wakajibu: “Saba.”^d **6** Naye akauagiza umati uketi chini. Kisha akachukua ile mikate saba, akatoa shukrani, akaimenga, na kuanza kuwapa wanafunzi wake waigawe, nao wakaugawia umati.^e **7** Walikuwa pia na samaki wachache wadogo, naye akawabariki, kisha akawaambia wawagawe hao pia. **8** Basi wakala wakashiba, kisha wakakusanya vipande vilivyobaki wakajaza vikapu saba vikubwa.^f **9** Kulikuwa na wanaume 4,000 hivi. Kisha Yesu akawaaga.

10 Mara moja akapanda mashua pamoja na wanafunzi wake akaenda eneo la Dalmanutha.^g **11** Akiwa huko Mafarisayo wakaja na kuanza kubishana naye, wakimtaka afanye ishara kutoka mbinguni, ili wamjaribu.^h **12** Kwa hiyo akahuzunika sana rohoni na kusema: “Kwa nini kizazi hiki kinatafuta ishara?”ⁱ Kwa kweli

8:3 * Au “wakiwa wamefunga.”

SURA YA 7

a Isa 35:5,6
Mt 15:31

SURA YA 8

b Mt 14:14
Mk 6:34

c Mt 15:32-38

d Mk 6:38

e Mk 6:41

f Mt 15:37

g Mt 15:39

h Mt 16:1-3

i Mt 12:38
Yoh 6:30

Safu ya 2

a Mt 16:4

b Mt 16:5-12

c Mt 16:6
Lu 12:1

d Mk 6:38

e Mt 14:20
Mk 6:43
Lu 9:17
Yoh 6:13

f Mt 15:37

g Mk 6:56

h Mt 7:32,33
Yoh 9:1,6

nasema, kizazi hiki hakitape-wa ishara yoyote.”^a **13** Ndipo akawaacha, akapanda mashua tena na kuvuka ng'ambo ya bahari.

14 Hata hivyo, walisahau kuchukua mikate na walikuwa na mkate mmoja tu katika mashua.^b **15** Naye akawao-nya waziwazi akisema: “Endeleeni kuwa macho; jihadharini na chachu* ya Mafarisayo na ya Herode.”^c **16** Basi wakaa-nza kubishana kati yao kwa sababu hawakuwa na mikate. **17** Yesu alipojua hilo, akawaambia: “Kwa nini mnabishana kuhusu kutokuwa na mikate? Je, bado hamjafahamu wala kuelewa? Je, bado mioyo yenu ni mizito isiweze kuelewa? **18** ‘Ingawa mna macho, kwa nini hamwoni; na ingawa mna masikio, kwa nini hamsikii?’ Je, hamkumbuki **19** nilipoimega ile mikate mitano^d kwa ajili ya wale wanaume 5,000, mlikusanya vipande vilivyobaki mkajaza vikapu vingapi?” Wakamwambia: “Kumi na viwili.”^e **20** “Nilipoimega ile mikate saba kwa ajili ya wale wanaume 4,000, mlikusanya vipande vilivyobaki mkajaza vikapu vikubwa vingapi?” Wakamwambia: “Saba.”^f **21** Ndipo akawauliza: “Je, bado hamjaelewa?”

22 Sasa wakafika Bethsaida. Watu wakamletea mwana-mume aliye kipofu, wakamsihi amguse.^g **23** Yesu akamshika mkono yule kipofu, akampeleka nje ya kijiji. Kisha akamtemea mate macho-ni,^h akaweka mikono juu yake na kumuuliza: “Je, unao-na kitu chochote?” **24** Yule

8:15 * Au “hamira.”

mtu akatazama juu na kusema: “Ninaona watu, lakini wanaonekana kama miti inayotembea.” **25** Akaweka tena mikono yake juu ya macho ya mtu huyo, naye akaona vizuri. Akawa tena na uwezo wa kuona, naye alikuwa akiona kila kitu waziwazi. **26** Basi akamwacha aende nyumbani, na kumwambia: “Usiingie kijijini.”

27 Yesu na wanafunzi wake wakaelekea kwenye vijiji vya Kaisaria Filipi, na wakiwa njiani, Yesu akaanza kuwauliza wanafunzi wake: “Watu wanasema mimi ni nani?”^a **28** Wakamjibu: “Yohana Mbatizaji,^b lakini wengine Eliya,^c na bado wengine mmoja wa manabii.” **29** Naye akawauliza: “Hata hivyo, ninyi mnasema mimi ni nani?” Petro akajibu: “Wewe ndiye Kristo.”^d **30** Ndipo akawaamuru wasimwambie mtu yeyote kumhusu.^e **31** Pia, akaanza kuwafundisha kwamba Mwana wa binadamu lazima apatwe na mateso mengi na kukataliwa na wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi, kisha atauawa,^f na baada ya siku tatu atafufuliwa.^g **32** Kwa kweli, alisema mambo hayo waziwazi. Lakini Petro akampeleka kando na kuanza kumkemea.^h **33** Yesu akageuka na kuwatazama wanafunzi wake, akamkemea Petro, akisema: “Nenda nyuma yangu, Shetani! kwa sababu hufikirii mawazo ya Mungu, bali ya wanadamu.”ⁱ

34 Sasa akauita umati na wanafunzi wake, akawaambia: “Mtu yeyote akitaka kunifuta, lazima ajikane mwenye-

SURA YA 8

a Mt 16:13-15
Lu 9:18, 19

b Mt 14:1, 2
Mk 6:14

c Mk 9:11

d Mt 16:16
Lu 9:20
Yoh 1:40, 41
Yoh 6:68, 69

e Mt 16:20
Mk 9:9
Lu 9:21, 22

f Mt 26:2

g Mt 16:21
Mt 17:22, 23

h Mt 16:22

i Mt 16:23

Safu ya 2

a Mt 10:38
Mt 16:24
Lu 9:23
Lu 14:27

b Mt 10:39
Mt 16:25
Lu 9:24
Yoh 12:25
Ufu 12:11

c Mt 16:26
Lu 9:25

d Zb 49:8

e Mt 10:33
Lu 9:26
Lu 12:9
2Ti 1:7, 8

f Mt 16:27
Mt 25:31
2Th 1:7

SURA YA 9

g Mt 16:28
Lu 9:27

h Mt 17:1-8
Lu 9:28-36

we, aubebe mti wake wa mateso* na aendelee kunifuata.^a **35** Kwa kuwa yeyote anayetaka kuokoa uhai wake ataupoteza,^{*} lakini yeyote anayepoteza uhai wake[#] kwa ajili yangu na kwa ajili ya habari njema atauokoa.^b **36** Kwa kweli, mtu atapata faida gani akiupata ulimwengu wote kisha apoteze uhai wake?^{#c} **37** Kwa kweli, mtu anaweza kutoa nini ili abadilishane na uhai wake?^{#d} **38** Kwa maana yeyote atakayenionea aibu mimi na maneno yangu katika kizazi hiki chenye uzinzi* na chenye dhambi, Mwana wa binadamu atamwonea aibu pia^e atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.”^f

9 Yesu akaendelea kusema: “Kwa kweli ninawaambia kwamba kuna baadhi ya wale waliosimama hapa ambao hawataonja kifo kamwe kabla ya kuona Ufalme wa Mungu ukiwa tayari umekuja katika nguvu.”^g **2** Siku sita baadaye Yesu akaenda pamoja na Petro, Yakobo, na Yohana kwenye mlima mrefu wakiva peke yao. Sura yake ikageuka mbele yao;^h **3** mavazi yake ya nje yakaanza kumetameta, yakawa meupe kuliko vile mfuaji nguo yeyote duniani angeweza kuyasafisha. **4** Pia, wakaona Eliya na Musa, wakizungumza na Yesu. **5** Kisha Petro akamwambia Yesu: “Rabi, ni vizuri sisi tuwe hapa. Basi, tutasimamisha mahema matatu,

8:34 * Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mti wa mateso.” **8:35** * Au “nafsi yake ataipoteza.” **8:35-37** # Au “nafsi yake.” **8:38** * Au “kisicho na uaminifu.”

moja lako, moja la Musa, na moja la Eliya.” **6** Kwa kweli, hakujua afanye nini, kwa maana walikuwa wameogopa sana. **7** Wingu likatokea na kuwafunika, na sauti^a ikasikika kutoka katika wingu wikuwa ikisema: “Huyu ni Mwanangu, mpendwa.”^b Msikilizeni.”^c **8** Kisha ghafla wakatazama huku na huku na hawakumwona tena mtu yeyote isipokuwa Yesu.

9 Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani, akawaamuru wasimwambie mtu yeyote kile walichoona,^d hadi Mwana wa binadamu atakapofufuliwa kutoka kwa wafu.^e **10** Wakayaweka maneno hayo moyoni,* lakini wakazungumza kati yao wenyewe kuhusu maana ya huko kufufuliwa kutoka kwa wafu. **11** Wakaanza kumuuliza: “Kwa nini waandishi husema kwamba lazima Eliya^f aje kwanza?”^g **12** Akawaambia: “Eliya anakuja kwanza na kurudisha mambo yote;^h lakini kwa nini imeandikwa kwamba lazima Mwana wa binadamu apatwe na mateso mengiⁱ na atendewe kwa dharau?”^j **13** Lakini ninawaambia kwamba kwa kweli, Eliya^k amekuja nao walimtendea kama walivyotaka, kama ilivyoandikwa kumhusu.”^l

14 Walipowakaribia wale wanafunzi wengine, wakaona umati mkubwa umewazunguka, na kulikuwa na waandishi waliokuwa wakibishana nao.^m **15** Lakini mara tu umati wote ulipomwona, ukashangaa, ukamkimbilia ili

9:10 *Au labda, “hawakumwambia mtu yeyote.”

SURA YA 9

a Lu 3:22
Yoh 12:28

b Zb 2:7
Isa 42:1
Mt 3:17
2Pe 1:17

c Kum 18:15
Mt 17:5
Lu 9:35
Mdo 3:22, 23

d Mt 12:15, 16
Mk 8:29, 30

e Mt 17:9
Lu 9:36

f Mal 4:5, 6
Mk 8:27, 28

g Mt 17:10

h Mt 17:11

i Da 9:26

j Zb 22:6, 7
Isa 50:6
Isa 53:3
Lu 23:11

k Mt 11:13, 14
Lu 1:13, 17

l Mt 17:12

m Lu 9:37

Safu ya 2

a Mt 17:14-17
Lu 9:38-42

b Kum 32:20

c Mt 17:17
Lu 9:41

d Mt 17:20
Mk 11:23
Lu 17:6
Yoh 11:40
Mdo 14:9, 10

e Lu 17:5

f Mt 17:18
Mk 1:23-25
Lu 4:34, 35
Mdo 10:38

kumsalimu. **16** Basi akawa-uliza: “Mnabishania nini?” **17** Mtu mmoja katika umati akamjibu: “Mwalimu, nilimleta mwanangu kwako kwa sababu ana roho anayemfanya awe bubu.”^a **18** Kila mara anapomshambulia humwangusha chini, naye hutoa povu mdomoni na kusaga meno yake na kuishiwa nguvu. Niliwaambia wanafunzi wako wamfukuze, lakini hawakuweza.” **19** Yesu akajibu: “Enyi kizazi kisicho na imani,^b nitaendelea kuwa pamoja nanyi mpaka lini? Nita-wavumilia mpaka lini? Mleteni hapa.”^c **20** Basi wakamleta yule mvulana kwa Yesu, lakini yule roho mwovu alipomwona, mara moja akamfanya yule mtoto agaegae. Baada ya kuanguka chini, akaendelea kujiviringisha, akitoa povu mdomoni. **21** Yesu akamuuliza baba yake: “Jambo hili limekuwa likitokea kwa muda gani?” Akasema: “Tangu utotoni, **22** naye humwangusha ndani ya moto na ndani ya maji ili amue. Lakini ikiwa unaweza kufanya chochote, tuhurumie na utusaidie.” **23** Yesu akamwambia: “Maneno hayo, ‘Ikiwa unaweza!’ Mambo yote yanawezekana kwa mtu mwenye imani.”^d **24** Mara moja baba ya yule mtoto akasema kwa sauti kubwa: “Nina imani! Nisaidie mahali ambapo ninahitaji imani!”^e

25 Yesu alipoona umati ukikusanyika haraka, akamkemea yule roho mwovu, akamwambia: “Wewe roho bubu na kiziwi, ninakuagiza umtoke mtoto huyu na usimwongie tena!”^f **26** Baada ya kupaza sauti na kugaagaa

sana, roho huyo akamtoka, na yule mtoto akaonekana ni kama amekufa, hivi kwamba watu wengi wakasema: "Ame-kufa!" **27** Lakini Yesu akamshika mkono na kumwinua, naye akasimama. **28** Baada ya kuingia ndani ya nyumba, wanafunzi wake wakamuuliza faraghani: "Kwa nini tulishi-ndwa kumfukuza?"^a **29** Aka-waambia: "Roho wa aina hii hawezi kutoka isipokuwa kwa sala."

30 Wakatoka huko wakapi-tia Galilaya, lakini hakuta-ka mtu yeyote ajue. **31** Kwa sababu alikuwa akiwafundi-sha wanafunzi wake na ku-waambia: "Mwana wa bi-nadamu atasalitiwa mikono-ni mwa watu, nao watumua,^b na ingawa atauawa, atafufu-ka baada ya siku tatu."^c **32** Hata hivyo, hawakulewa maneno aliyosema, nao walio-gopa kumuuliza.

33 Nao wakaingia Kaper-naumu. Alipokuwa ndani ya nyumba akawauliza: "Mliku-wa mkibishania nini baraba-rani?"^d **34** Wakakaa kimya, kwa maana barabarani wali-kuwa wakibishana kuhusu ali-ye mkuu kati yao. **35** Basi akaketi na kuwaita wale 12 akawaambia: "Yeyote ana-yetaka kuwa wa kwanza, la-zima awe wa mwisho kati ya wote na mhudumu wa wote."^e **36** Kisha akamchukua mto-to mdogo, akamsimamisha ka-tikati yao; akamkumbatia na kuwaambia: **37** "Yeyote anayempokea mtoto mdogo^f kama huyu kwa msingi wa jina langu ananipokea mimi pia; na yeyote anayenipokea mimi hanipokei mimi tu, bali pia Yule aliyenituma."^g

SURA YA 9

a Mt 17:19, 20

b Mt 26:2

c Mt 16:21
Mt 17:22, 23
Mk 8:31
Lu 9:44, 45d Mt 18:1-5
Lu 9:46-48
Lu 22:24e Mt 20:26-28
Mk 10:43-45
Flp 2:8, 9

f Lu 18:16

g Mt 10:40
Lu 9:48
Yoh 13:20

Safu ya 2

a Lu 9:49

b Lu 9:50

c Mt 25:40

d Mt 10:42

e Mt 18:6
Lu 17:1, 2f Mt 5:30
Mt 18:8
Kol 3:5g Mt 10:28
Mt 23:33
Lu 12:5

h Gal 5:24

i Mt 5:29
Mt 18:9
Ro 8:13

38 Yohana akamwambia: "Mwalimu, tulimwona mtu fu-lani akifukuza roho waovu kwa kutumia jina lako, tukaja-ribu kumzuia, kwa sababu ha-kuwa akitufuata."^a **39** Laki-ni Yesu akasema: "Msijaribu kumzuia, kwa maana haku-na yeyote atakayefanya ma-tendo yenye nguvu kwa msi-ngi wa jina langu atakayeweza kusema mambo mabaya kuni-husu. **40** Kwa maana yeyote ambaye hatupingi yuko upa-nde wetu.^b **41** Na yeyote anayewapa kikombe cha maji ya kunywa kwa sababu ninyi ni wa Kristo,^c kwa kweli nina-waambia hatapoteza kamwe thawabu yake.^d **42** Lakini ye-yote anayemkwaza mmoja wa hawa wadogo walio na imani, ingekuwa afadhali ikiwa jiwe la kusagia ambalo huzungu-shwa na punda lingefungwa shingoni mwake kisha atupwe baharini.^e

43 "Ikiwa mkono wako una-kufanya ukwazike, ukate. Ni afadhali uingie katika uzima ukiwa kilema kuliko kuingia ukiwa na mikono miwili katika Gehena,* katika moto usiowe-za kuzimwa.^f **44** *— **45** Na ikiwa mguu wako unakufanya ukwazike, ukate. Ni afadhali uingie katika uzima ukiwa ki-lemu kuliko kutupwa katika Gehena* ukiwa na miguu mi-wili.^g **46** *— **47** Na ikiwa jicho lako linakufanya ukwazi-ke, litupe mbali.^h Ni afadhali uingie katika Ufalme wa Mu-ngu ukiwa na jicho moja ku-liko kutupwa katika Gehena ukiwa na macho mawili,ⁱ

9:43, 45, 47 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 9:44, 46 *Angalia Nyo-ngeza A3.

48 mahali ambapo funza hawafi na moto hauzimwi.^a

49 “Kwa maana kila mtu lazima atiwe chumvi kwa moto.”^b

50 Chumvi ni nzuri, lakini ikipoteza ladha yake, mtaikoleza na nini?^c Iweni na chumvi ndani yenu,^d na mdumishe amani kati yenu.”^e

10 Alipotoka hapo akaenda kwenye mipaka* ya Yudea, ng’ambo ya Yordani, na umati ukakusanyika tena karibu naye. Kama kawaida yake, akaanza tena kuwafundisha.^f **2** Mafarisayo wakaaja, wakikusudia kumjaribu, wakamuuliza kama ni halali kwa mwanamume kumtaliki mke wake.^g **3** Akawajibu: “Musa aliwapa amri gani?” **4** Wakasema: “Musa aliruhusu kumwandikia cheti cha kumfukuza na kumtaliki.”^h **5** Lakini Yesu akawaambia: “Aliwaandikia amri hiyo kwa sababu ya ugumu wa miyo yenu.”ⁱ **6** Hata hivyo, tangu mwanzo wa uumbaji ‘Aliwaumba mwanamume na mwanamke.^k **7** Kwa sababu hiyo, mwanamume atamwacha baba yake na mama yake,^l **8** na hao wawili watakuwa mwili mmoja,^m basi wao si wawili tena, bali mwili mmoja. **9** Kwa hiyo, kile ambacho Mungu ameunganisha, mtu yeyote asikitenganishe.”ⁿ **10** Walipoingia tena ndani ya nyumba wanafunzi wakaanza kumuuliza kuhusu jambo hilo. **11** Akawaambia: “Yeyote anayemtaliki mke wake na kumwoa mwingine anafanya uzinzi^o dhidi yake, **12** na ikiwa mwanamke baada ya kumta-

10:1 *Au “karibu na mipaka.”

SURA YA 9

- a Isa 66:24
b Lu 17:29
c Mt 5:13
Lu 14:34, 35
d Kol 4:6
e Ro 12:18
Efe 4:29
1Th 5:13
Ebr 12:14

SURA YA 10

- f Mt 19:1, 2
g Mt 19:3
h Kum 24:1
Mt 5:31
Mt 19:7
i Mt 19:8
j Kum 9:6
Mdo 13:18
k Mwa 1:27
Mwa 5:2
Mt 19:4
l Mt 19:5
m Mwa 2:24
Efe 5:31
n Mt 19:6
o Mt 5:32
Mt 19:9
Lu 16:18

Safu ya 2

- a Ro 7:3
b Mt 19:13
Lu 18:15
c Mt 18:4
Mt 19:14
Lu 18:16
1Pe 2:2
d Mt 18:3
Lu 18:17
e Mk 9:36
f Mt 19:16
Lu 18:18
g Zb 86:5
Mt 19:17
Lu 18:19
h Kut 20:13
Kum 5:17
Mt 5:21
1Yo 3:15
i Kut 20:14
Kum 5:18
j Kut 20:15
Kum 5:19
k Kut 20:16
Kum 5:20
l Law 19:13
m Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:2
n Mt 19:21
o Lu 18:23

liki mume wake anaolewa na mwingine, anafanya uzinzi.”^a

13 Watu wakaanza kumletea watoto wadogo ili awaguse, lakini wanafunzi wakawa-kemea.^b **14** Alipoona hivyo, Yesu akakasirika na kuwaambia: “Waacheni watoto wadogo waje kwangu; msijaribu kuwazuia, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa wale walio kama hao.”^c **15** Kwa kweli ninawaambia, yeyote asiyeupokea Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hataingia kamwe ndani yake.”^d **16** Akawachukua watoto akawakumbatia na kuanza kuwabariki, akiweka mikono yake juu yao.^e

17 Alipokuwa akiondoka, mwanamume fulani akakim-bilia, akapiga magoti mbele yake na kumuuliza: “Mwalimu Mwema, ninapaswa kufanya nini ili niurithi uzima wa milele?”^f **18** Yesu akamwambia: “Kwa nini unaniita mwema? Hakuna aliye mwema, isipokuwa mmoja, Mungu.”^g **19** Unazijua amri hizi: ‘Usiue,^h usifanye uzinzi,ⁱ usiibe,^j usitoe ushahidi wa uwongo,^k usipunje,^l mheshimu baba yako na mama yako.”^m **20** Mtu huyo akamwambia: “Mwalimu, nimeyashika mambo hayo yote tangu nilipokuwa kijana.” **21** Yesu akamtazama, akampenda na kumwambia: “Bado unahitaji kufanya jambo moja: Nenda ukauze vitu ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha uje uwe mfua-si wangu.”ⁿ **22** Lakini akasikitishwa na jibu hilo, akaenda zake akiwa na huzuni, kwa maana alikuwa na mali nyingi.^o

23 Yesu akatazama huku na huku na kuwaambia wanafunzi wake: “Itakuwa vigumu sana kwa wale walio na pesa kuingia katika Ufalme wa Mungu!”^a **24** Lakini wanafunzi wakashangazwa na maneno yake. Naye Yesu akawaambia: “Wanangu, ni vigumu sana kuingia katika Ufalme wa Mungu! **25** Ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu.”^b **26** Wakazidi kushangaa wakaambia: * “Ni nani anayeweza kuokolewa?”^c **27** Akatazama moja kwa moja na kusema: “Kwa wanadamu haiwezekani, lakini sivyo ilivyo kwa Mungu, kwa maana mambo yote yanawezekana kwa Mungu.”^d **28** Petro akaanza kumwambia: “Tazama! Tumeacha kila kitu na kukufuata.”^e **29** Yesu akasema: “Kwa kweli ninawaambia, hakuna mtu aliyecha nyumba au ndugu au dada au mama au baba au watoto au mashamba kwa ajili yangu na kwa ajili ya habari njema^f **30** ambaye hatapata mara 100 sasa katika kipindi hiki—nyumba, ndugu, dada, mama, watoto, mashamba, pamoja na mateso^g—na katika mfumo wa mambo* unaokuja, uzima wa milele. **31** Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na wa mwisho watakuwa wa kwanza.”^h **32** Sasa walikuwa barabarani wakipanda kwenda Yerusalemu, Yesu alikuwa akiwatangulia, nao walikuwa wameshangaa, lakini wale waliofuata wakaanza kuogopa.

10:26 *Au labda, “wakaambiana.”
10:30 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 10

a Yer 9:23
ITI 6:17

b Mt 19:24
Lu 18:25

c Mt 19:25, 26
Lu 18:26, 27

d Ayu 42:2

e Mt 19:27
Lu 18:28

f Mt 10:37
Mt 19:29
Lu 18:29, 30

g Mt 5:11
Mdo 14:22

h Mt 19:30
Mt 20:16
Lu 13:30

Safu ya 2

a Mt 20:17-19
Mk 8:31
Mk 9:31
Lu 9:22
Lu 18:31-33

b Mdo 10:40
Iko 15:3, 4

c Mt 10:2

d Mt 20:20, 21

e Mt 19:28

f Mt 20:22, 23
Lu 12:50
Yoh 18:11
Ro 6:3

g Mdo 12:2
Ufu 1:9

h Mt 20:24

Akawapeleka kando tena wale 12 na kuanza kuwaambia mambo yaliyokuwa karibu kumpata:^a **33** “Tazama! Tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana wa binadamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi. Nao watamhukumia kifo na kumtia mikononi mwa watu wa mataifa, **34** nao watamdhihaki, watamtemea mate, watampiga mijeledi na kumuua, lakini baada ya siku tatu atafufuka.”^b

35 Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo,^c wakaenda na kumwambia: “Mwalimu, tunataka utufanyie chochote tutakachokuomba.”^d **36** Akawauliza: “Mnataka niwafanyie nini?” **37** Wakamwambia: “Turuhusu tuketi, mmoja upande wako wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto, katika utukufu wako.”^e

38 Lakini Yesu akawaambia: “Hamjui kile mnachoomba. Je, mnaweza kunywa kikombe ambacho ninakunywa au kubatizwa kwa ubatizo ninaobatizwa?”^f **39** Wakamwambia: “Tunaweza.” Ndipo Yesu akawaambia: “Kikombe ninachokunywa mtakunywa, na ubatizo ninaobatizwa mtabatizwa.”^g **40** Hata hivyo, kuketi upande wangu wa kuume au wa kushoto sina haki ya kutoa, bali wataketi wale ambao wametayarishiwa.”

41 Wale wengine kumi waliliposikia jambo hilo, wakawakasirikia Yakobo na Yohana.^h

42 Lakini Yesu akawaita akawaambia: “Mnajua kwamba wale wanaotawala* matai-

10:42 *Au “wanaoonwa kuwa watawala wa.”

fa hupiga ubwana juu yao na wakuu wao hutumia mamlaka juu yao.^a **43** Haipaswi kuwa hivyo kati yenu; lakini yeyote anayetaka kuwa mkubwa kati yenu lazima awe mhudumu wenu,^b **44** na yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kati yenu lazima awe mtumwa wa wote. **45** Kwa maana hata Mwana wa binadamu alikuja, si kuhudumiwa, bali kuhudumu^c na kutoa uhai wake uwe* fidia badala ya wengi.”^d

46 Kisha wakafika Yeriko. Lakini yeye na wanafunzi wake na umati mkubwa walipokuwa wakitoka Yeriko, Bartimayo (mwana wa Timayo), kipofu aliyekuwa akiombao- mba, alikuwa ameketi kando ya barabara.^e **47** Aliposikia kwamba ni Yesu Mnazareti, akaanza kusema kwa sauti kubwa: “Mwana wa Daudi,^f Yesu, nihurumie!”^g **48** Ndipo wengi wakaanza kumkemea, wakimwambia anyamaze, lakini akazidi kusema kwa sauti kubwa: “Mwana wa Daudi, nihurumie!”^g **49** Basi Yesu akasimama na kusema: “Mwitieni.” Nao wakamwita yule kipofu, wakamwambia: “Jipe moyo! Simama; anakuita.” **50** Akatupa vazi lake la nje, akasimama haraka na kumwendea Yesu. **51** Kisha Yesu akamwuliza: “Unataka nikufanyie nini?” Yule kipofu akamwambia: “*Raboni*,* naomba niweze kuona tena.” **52** Yesu akamwambia: “Nenda, imani yako imekuponya.”^h Na mara moja akaanza kuona, na naye akaanza kumfuata barabarani.

10:45 *Au “nafsi yake iwe.” **10:47, 48** *Au “nionyeshe rehema!” **10:51** *Maana yake “Mwalimu.”

SURA YA 10

a Mt 20:25
Lu 22:25
1Pe 5:2, 3

b Mt 20:26, 27
Mk 9:35
Lu 9:48
Lu 22:26

c Yoh 13:14
Flp 2:7

d Isa 53:10
Da 9:24
Mt 20:28
Gal 3:13
Tit 2:13, 14

e Mt 20:29-34
Lu 18:35-43

f Yer 23:5
Ro 1:3

g Mt 9:27
Mt 15:22

h Mt 9:20, 22

i Isa 35:5
Isa 42:7
Mk 8:25

Safu ya 2

SURA YA 11

a Yoh 11:18

b Mt 21:1-3
Lu 19:29-34

c Mt 21:6

d 1Fa 1:33
Zek 9:9

e Mt 21:7, 8
Yoh 12:14, 15

f Lu 19:36
Yoh 12:13

g Mt 21:15

h Zb 118:25, 26
Mt 21:9
Lu 19:37, 38
Yoh 12:13

i Zek 9:9
Lu 1:32

11 Walipokuwa wakikaribia Yerusalemu, Bethfage na Bethania^a kwenye Mlima wa Mizeituni, akawatuma wawili kati ya wanafunzi wake,^b **2** akawaambia: “Nendeni katika kijiji mtakachokiona, na mara tu mtakapochingia mtamwona mwanapunda akiwa amefungwa, ambaye hakuna mtu amewahi kuketi juu yake. Mfungueni na kumleta. **3** Mtu yeyote akiwauliza, ‘Kwa nini mnamfungua?’ mwambieni, ‘Bwana anamhitaji, na atamrudisha hapa mara moja.’” **4** Basi wakaeenda na kumpata mwanapunda akiwa amefungwa kwenye mlango, karibu na barabara, nao wakamfungua.^c **5** Lakini watu waliokuwa wamesimama hapo wakawauliza: “Kwa nini mnamfungua mwanapunda huyu?” **6** Wakajibu kama Yesu alivyowaambia, nao wakawaacha waende.

7 Wakampelekea Yesu huyo mwanapunda,^d wakatandika mavazi yao ya nje juu yake, naye akaketi juu yake.^e **8** Pia, wengi wakatandaza mavazi yao ya nje barabarani, lakini wengine wakatandaza matawi ya miti waliyokata katika mashamba.^f **9** Watu waliokuwa mbele na wale waliofuata nyuma wakaendelea kupaza sauti: “Tunaomba umwokoe!^g Amebarikiwa yule anayekuja katika jina la Yehova!”^h **10** Umebarikiwa Ufalme unaokuja wa baba yetu Daudi!ⁱ Tunaomba umwokoe, katika vilele vilivyo juu!” **11** Akaingia Yerusalemu na kwenda hekaluni, akatazama vitu vyote huku na

11:9 *Angalia Nyongeza A5.

huku, lakini kwa kuwa muda ulikuwa umesonga sana, akaenda Bethania pamoja na wale 12.^a

12 Siku iliyofuata, walipokuwa wakitoka Bethania, akahisi njaa.^b **13** Akaona kwa mbali mtini wenye majani, akaenda kuona kama angepata chochote. Lakini, alipoufikia, hakupata chochote ila majani, kwa maana hayakuwa majira ya tini. **14** Basi akauambia: "Mtu yeyote asile matunda yako tena kamwe."^c Nao wanafunzi wake walikuwa wakisikiliza.

15 Wakafika Yerusalemu. Akaingia hekaluni akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, naye akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadili pesa na viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa.^d **16** na hakumruhusu mtu yeyote apite hekaluni akiwa amebeba chombo. **17** Alikuwa akiwafundisha akisema: "Je, haikuandikwa, 'Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa ajili ya mataifa yote?'"^e Lakini mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi."^f **18** Wakuu wa makuhani na waandishi waliposikia hayo, wakaanza kutafuta njia ya kumuua;^g kwa maana walimwogopa, kwa sababu umati wote ulishangaza na mafundisho yake.^h

19 Ilipofika jioni, wakatoka jijini. **20** Lakini walipokuwa wakipita asubuhi na mapema, wakaona ule mtini ukiwa umenyauka kuanzia kwenye mizi-zi.ⁱ **21** Petro, akaukumbuka na kumwambia: "Rabi, ona! ule mtini ulioulaani umenyauka."^j **22** Yesu akawaambia:

SURA YA 11

a Mt 21:10

b Mt 21:18

c Mt 21:19
Mk 11:20

d Mt 21:12
Lu 19:45, 46
Yoh 2:14-16

e 1Fa 8:43
Isa 56:7

f Yer 7:11
Mt 21:13
Lu 19:46
Yoh 2:16

g Mk 14:1
Lu 20:19

h Lu 19:47, 48

i Mt 21:19, 20

j Mk 11:14

Safu ya 2

a Mt 17:20
Mt 21:21
Lu 17:6

b Mt 7:7
Mt 18:19
Mt 21:22
Lu 11:9
Yoh 14:13
Yoh 15:7
Yoh 16:24

c Zb 103:10-12
Mt 6:12, 14
Efe 4:32
Kol 3:13

d Mt 21:23-27
Lu 20:1-8

e Mk 1:4

f Mt 21:25
Lu 20:4

g Mt 3:1, 5
Mt 14:3, 5
Mk 6:20

"Iweni na imani katika Mungu. **23** Kwa kweli ninawaambia mtu yeyote anayeuambia mlima huu, 'Ng'oka, ukatupwe baharini,' bila kuwa na shaka moyoni mwake lakini awe na imani kwamba yale anayosema yatatukia, itakuwa hivyo."^a **24** Ndiyo sababu ninawaambia, mambo yote mnayosali na kuomba, iweni na imani kwamba mmeyapokea, nanyi mtayapata.^b **25** Na mnaposimama kusali, wasameheni watu makosa waliyowatendea; ili Baba yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi makosa yenu pia."^c **26** *—

27 Wakaja tena Yerusalemu. Na alipokuwa akitembea hekaluni, wakuu wa makuhani, waandishi, na wazee wakaja **28** na kumuuliza: "Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Au ni nani aliye kupa mamlaka ya kufanya mambo haya?"^d **29** Yesu akawaambia: "Nitawauliza swali moja. Mkinijibu, nitawaambia ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani. **30** Je, ubatizo wa Yohana^e ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?* Nijibuni."^f **31** Basi wakaanza kujadiliana kati yao, wakisema: "Tukisema, 'Ulitoka mbinguni,' atatuuliza, 'Basi, kwa nini hamkumwamini?' **32** Lakini je, tutathubutu kusema, 'Ulitoka kwa wanadamu?'" Kwa kuwa waliogopa umati, kwa maana umati wote uliamini kwa kweli Yohana alikuwa nabii.^g **33** Basi wakamjibu Yesu: "Hatujui."

11:26 *Angalia Nyongeza A3. 11:30 *Au "chanzo chake ni wanadamu?"

Naye Yesu akawaambia: “Nami siwaambii ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani.”

12 Akaanza kusema nao kwa mifano: “Mtu fulani alipanda shamba la mizabibu^a akalizungushia ua, akachimba shinikizo la divai, akajenga mnara,^b kisha akalikodisha kwa wakulima, naye akasafiri kwenda ng’ambo.^c **2** Majira yalipofika akamtuma mtumwa kwa wakulima ili achukue kutoka kwao baadhi ya matunda ya shamba la mizabibu. **3** Lakini wakamkamata, wakampiga na kumfukuza mikono mitupu. **4** Akamtuma tena mtumwa mwingine kwao, na huyo wakampiga kichwani na kumwaibisha.^d **5** Akamtuma mwingine, na huyo wakamuua, akawatuma wengine wengi, wakawapiga baadhi yao na kuwaua wengine. **6** Alikuwa na mmoja zaidi, mwana wake mpendwa.^e Mwishowe akamtuma kwao akisema: ‘Watamheshimu mwangu.’ **7** Lakini wakulima wakaambiana, ‘Huyu ndiye mriti.’^f Njooi tumuue, na urithi utakuwa wetu.’ **8** Kwa hiyo wakamkamata, wakamuua na kumtupa nje ya shamba la mizabibu.^g **9** Mwenye shamba la mizabibu atafanya nini? Atakuja na kuwaua wakulima hao, kisha atawapa watu wengine shamba hilo la mizabibu.^h **10** Je, hamkusoma kamwe andiko hili: ‘Jiwe ambalo wajenzi walilikataa, limekuwa jiwe kuu la pembeni.’ⁱ **11** Hili limetoka kwa Yehova,* na ni lenye kustaajabisha machoni petu?”^j

12:10 *Tnn., “kichwa cha pembeni.”
12:11 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 12

a Isa 5:7

b Isa 5:2

c Mt 21:33-41
Lu 20:9-16

d Ebr 11:32, 37

e Zb 2:7
Gal 4:4
1Yo 4:9

f Zb 2:8
Ebr 1:2

g Mdo 2:23

h Mt 21:41, 43

i Mt 21:42
Lu 20:17
Mdo 4:10, 11
Efe 2:20
1Pe 2:7

j Zb 118:22, 23

Safu ya 2

a Mt 21:45, 46
Lu 20:19

b Mt 22:15-22
Lu 20:20-26

c Ro 13:7
Tit 3:1
1Pe 2:13

d Mal 3:8
Mt 22:21
Lu 20:25

e Mdo 23:8

f Mt 22:23-28
Lu 20:27-33

g Mwa 38:7, 8
Kum 25:5, 6

12 Ndipo wakataka kumkamata, lakini waliuogopa umati, kwa maana walijua kwamba mfano aliosema uliwahusu. Basi wakamwacha na kwenenda zao.^a

13 Kisha wakawatuma baadhi ya Mafarisayo na wafuasi wa chama cha Herode ili wamnase kwa maneno yake.^b

14 Walipofika wakamwambia: “Mwalimu, tunajua wewe husema ukweli na hutafuti kibaali cha yeyote, kwa maana huanjali sura ya nje ya mtu, bali unafundisha njia ya Mungu kupatana na kweli. Je, ni halali* au si halali kumlipa Kaisari kodi?”[#] **15** Je, tunapaswa kulipa, au hatupaswi kulipa? Akagundua unafiki wao, akawaambia: “Kwa nini mnanijaribu? Nileteeni dinari* nitazame.” **16** Wakaleta dinari moja, akawauliza: “Sura hii na maandishi haya ni ya nani?” Wakajibu: “Ni ya Kaisari.” **17** Ndipo Yesu akasema: “Mlipeni Kaisari vitu vya Kaisari,^c na Mungu vitu vya Mungu.”^d Nao wakashangazwa naye.

18 Sasa Masadukayo, ambao husema hakuna ufufuo,^e wakaja na kumuuliza:^f **19** “Mwalimu, Musa alitundikia kwamba mtu akifa na kuacha mke lakini hakuacha mtoto, ndugu yake anapaswa kumchukua mke huyo ili kumwinulia ndugu yake uzao.^g **20** Kulikuwa na ndugu saba. Wa kwanza alioa mwanamke, lakini alipokufa hakuacha uzao wowote. **21** Wa pili akamwoa, lakini akafa bila kuacha uzao, na wa tatu vivyo hivyo. **22** Na wote saba hawakuacha uzao.

12:14 *Au “ni sawa.” #Au “kodi ya kichwa.” 12:15 *Angalia Nyongeza B14.

Mwishowe pia yule mwana-
mke akafa. **23** Katika ufufuo
atakuwa mke wa nani? Kwa
maana wote saba walikuwa
wamemwoa.” **24** Yesu aka-
waambia: “Ninyi mmeko-
sea kwa sababu hamjui Ma-
ndiko wala nguvu za Mungu.^a
25 Kwa maana wanapofufu-
liwa kutoka kwa wafu, wanau-
me hawaoi wala wanawake ha-
waolewi, bali wao ni kama
malaika mbinguni.^b **26** Laki-
ni kuhusu kufufuliwa kwa
wafu, je, hamkusoma katika
kitabu cha Musa, simulizi ku-
husu kile kichaka cha miiba
kwamba Mungu alimwambia:
‘Mimi ni Mungu wa Abrahama
na Mungu wa Isaka na Mun-
gu wa Yakobo?’^c **27** Yeye si
Mungu wa wafu, bali wa walio
hai. Mmekosea sana.”^d

28 Mmoja kati ya waandi-
shi waliokuwa wamekuja na
kusikia wakibishana, akijua
kwamba alikuwa amewajibu
vizuri, akamuuliza: “Ni amri
gani iliyo ya kwanza* kati ya
zote?”^e **29** Yesu akajibu: “Ya
kwanza ni hii, ‘Sikilizeni,
enyi Waisraeli, Yehova* Mun-
gu wetu ni Yehova* mmoja,
30 nawe lazima umpende Ye-
hova* Mungu wako kwa moyo
wako wote na kwa nafsi# yako
yote na kwa akili yako yote na
kwa nguvu zako zote.’^f **31** Ya
pili ni hii, ‘Lazima umpende
jirani yako kama unavyojipe-
nda mwenyewe.’^g Hakuna
amri nyingine iliyo kubwa ku-
liko amri hizi.” **32** Yule mwa-
ndishi akamwambia: “Mwali-
mu, umesema vema kupatana
na kweli, ‘Yeye ni Mmoja, na

12:28 *Au “muhimu zaidi.” 12:29, 30,
36 *Angalia Nyongeza A5. 12:30
#Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 12

- a Mt 22:29
- b Mt 22:30
Lu 20:34-36
- c Kut 3:2, 6
Mt 22:31
Lu 20:37
- d Mt 22:32
Lu 20:38
- e Mt 22:34-36
- f Kum 6:4, 5
Yos 22:5
Mt 22:37
Lu 10:27
- g Law 19:18
Mt 22:39, 40
Ro 13:9
Gal 5:14
Yak 2:8

Safu ya 2

- a Kum 4:39
Kum 6:4
Isa 45:21
- b Kum 6:5
1Sa 15:22
Ho 6:6
- c Mt 22:46
- d Mt 22:42-45
Lu 20:41-44
Yoh 7:42
- e 2Sa 23:2
2Ti 3:16
2Pe 1:21
- f Zb 110:1
Mdo 2:34, 35
1Ko 15:25
Ebr 1:13
- g Ro 1:3
Ufu 22:16
- h Lu 20:45-47
- i Mt 23:6, 7
Lu 11:43

hakuna mwingine isipokuwa
yeye’;^a **33** na kumpenda Mun-
gu kwa moyo wote na kwa
uelewaji wote na kwa nguvu
zote na pia mtu kumpenda ji-
rani yake kama anavyojipenda
mwenyewe ni bora kuliko ma-
toleo yote mazima ya kuteke-
tezwa na dhabihu.”^b **34** Yesu
alipotambua kwamba ameji-
bu kwa kutumia akili, aka-
mwambia: “Wewe huko mbali
na Ufalme wa Mungu.” Lakini
hakuna mtu aliyethubutu tena
kumuuliza swali.^c

35 Hata hivyo, Yesu akie-
ndelea kufundisha hekaluni,
akawauliza: “Kwa nini waandi-
shi husema kwamba Kristo ni
mwana wa Daudi?^d **36** Kupi-
tia roho takatifu^e Daudi mwe-
nyewe alisema, ‘Yehova* ali-
mwambia Bwana wangu: “Keti
kwenye mkono wangu wa kuu-
me mpaka niwaweke maadui
wako chini ya miguu yako.”’^f
37 Daudi mwenyewe anamwi-
ta Bwana, basi Kristo anawe-
zaje kuwa mwanawe?”^g

Na umati mkubwa uliku-
wa ukimsikiliza kwa fura-
ha. **38** Akaendelea kufundi-
sha akisema: “Jihadharini na
waandishi kwa kuwa wanape-
nda kutembea wakiwa wame-
vaa kanzu na wanapenda ku-
salimiwa sokoni^h **39** na viti
vya mbele* katika masinago-
gi na mahali penye heshi-
ma zaidi kwenye milo ya jio-
ni.ⁱ **40** Wao ndio wanaomali-
za nyumba* za wajane na ku-
toa sala ndefu ili waonekane.[#]
Hao watapea hukumu kali
zaidi.”^Δ

12:39 *Au “mahali bora.” 12:40 *Au
“mali.” #Au “kujifanya.” ΔAu “wata-
pokea hukumu nzito.”

41 Kisha akaketi akitazama masanduku* ya hazina^a na kuanza kuangalia jinsi umati ulivyokuwa ukitumbukiza pesa katika masanduku hayo, na matajiri wengi walikuwa wakitumbukiza sarafu nyingi.^b **42** Mjane fulani maskini akaja akatumbukiza sarafu mbili ndogo zenye thamani ndogo sana.*^c **43** Basi akawaita wanafunzi wake na kuwaambia: “Kwa kweli nina-
waambia mjane huyu maskini ametumbukiza zaidi ya wote waliotumbukiza pesa ndani ya masanduku ya hazina.^d **44** Kwa maana wote walitumbukiza kutokana na ziada yao, lakini yeye, ingawa ni maskini,* alitumbukiza kila kitu alichokuwa nacho, riziki yake yote.”^e

13 Alipokuwa akitoka hekaluni mmoja wa wanafunzi wake akamwambia: “Mwalimu, ona! jinsi mawe na majengo haya yalivyo maridadi!”^f **2** Hata hivyo, Yesu akamwambia: “Unayaona majengo haya makubwa? Hakuna jiwe litakaloachwa hapa juu ya jiwe lingine bila kuangu-shwa chini.”^g

3 Alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni, huku hekalu likiwa linaonekana, Petro, Yakobo, Yohana, na Andrea wakamuuliza faraghani: **4** “Tuambie, mambo haya yatatukia lini, na ni nini itakayokuwa ishara ya wakati ambapo mambo haya yatafikia mwisho?”^h **5** Basi Yesu akaanza kuwaambia: “Jiha-

12:41 *Au “makasha.” 12:42 *Tnn., “leptoni mbili, ambazo ni kwadrani moja.” Angalia Nyongeza B14. 12:44 *Au “ana uhitaji.”

SURA YA 12

a 2Fa 12:9

b Lu 21:1

c Lu 21:2

d Lu 21:3
2Ko 8:12

e Lu 21:4

SURA YA 13

f Mt 24:1
Lu 21:5g Law 26:31
Mt 24:2
Lu 19:44
Lu 21:6h Mt 24:3
Lu 21:7

Safu ya 2

a Mt 24:4, 5
Lu 21:8b Mt 24:6
Lu 21:9

c Ufu 6:4

d Mt 24:7
Lu 21:10, 11
Ufu 6:6, 8

e Mt 24:8

f Mdo 4:15

g Mt 10:17
Yoh 16:2h Mt 24:9
Lu 21:12, 13
2Ti 3:12
Ufu 2:10i Mt 24:14
Ro 10:18
Ufu 14:6j Kut 4:12
Mt 10:19, 20
Lu 12:11, 12
Lu 21:14, 15
Mdo 4:8
Mdo 6:9, 10k Mik 7:6
Mt 10:21
Lu 21:16
2Ti 3:1, 3

l Lu 21:17

m 2Ti 4:7
Ebr 3:6n Mt 10:22
Mt 24:13
Lu 21:19
Ufu 2:10o Da 9:27
Da 11:31

dharini ili mtu yeyote asiwapotoshe.^a **6** Wengi watakuja kwa msingi wa jina langu, wakisema, ‘Mimi ndiye,’ nao watawapotosha wengi. **7** Zaidi ya hayo, mtakaposikia kuhusu vita na habari za vita, msioogope; lazima mambo hayo yatukie, lakini ule mwisho bado.^b

8 “Kwa maana taifa litapigana na taifa na ufalme kupigana na ufalme;^c kutakuwa na matememeko ya ardhii sehemu mbalimbali; pia kutakuwa na upungufu wa chakula.^d Mambo hayo ni mwanzo wa maumivu ya taabu.^e

9 “Lakini ninyi jihadhari ni. Watu watawapeleka mahakamani,^f nanyi mtapigwa katika masinagogi^g na kusimamishwa mbele ya magavana na wafalme kwa ajili yangu, ili kuwa ushahidi kwao.^h

10 Pia, katika mataifa yote, lazima habari njema ihubiriwe kwanza.ⁱ **11** Na watakapokuwa wakiwapeleka kuwashtaki, msihangaikie kuhusu jambo mtakalosema; bali semeni jambo mtakalopewa saa hiyo, kwa maana si ninyi mnaosema, bali ni roho takatifu.^j **12** Isitoshe, ndugu atamtoa ndugu yake ili auawe, na baba atamtoa mtoto, na watoto watainuka dhidi ya wazazi na kufanya wauawe.^k **13** Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa sababu ya jina langu.^l Lakini yule atakayevumilia* mpaka mwisho^m ndiye atakayeokolewa.ⁿ

14 “Hata hivyo, mtakapoo-na kile kitu chenye kuchukiza sana kinachosababisha ukiwa^o kikiwa kimesimama

13:13 *Au “anayevumilia.”

mahali ambapo hakipaswi kuwa (msomaji na atumie utambuzi), ndipo wale walio Yudea waanze kukimbilia milimani.^a **15** Mtu aliye juu ya paa la nyumba asishuke wala asiingie kuchukua kitu chochote ndani ya nyumba yake; **16** na mtu aliye shambani asirudi kwenye vitu vilivyo nyuma ili kuchukua vazi lake la nje. **17** Ole wao wanawake wenyewe mimba na wale wanaonyesha mtoto katika siku hizo!^b **18** Endeeleni kusali kwamba isitukie wakati wa majira ya baridi kali; **19** kwa maana siku hizo zitakuwa za dhiki^c ambayo haijawahi kutokea tangu mwanzao wa uumbaji ambao Mungu aliumba mpaka wakati huo, na haitatokea tena.^d **20** Kwa kweli, kama Yehova* hangezifupisha siku hizo, hakuna mwili wowote ambao ungeokolewa. Lakini kwa sababu ya wale waliochaguliwa ambao amewachagua, amezifupisha siku hizo.^e

21 "Pia, mtu yeyote akiwaambia, 'Tazama! Kristo yuko hapa,' 'Tazama! yuko pale,' msiamini.^f **22** Kwa maana Kristo wengi wa uwongo na manabii wa uwongo^g watatokea na kufanya ishara na majabu ili kuwapotosha, ikiwezekana, hata wale waliochaguliwa. **23** Basi, jihadharini.^h Nimewaambia mambo yote mapema.

24 "Lakini katika siku hizo, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa nuru yake,ⁱ **25** nazo nyota zitakuwa zikianguka kutoka mbinguni na nguvu zi-

SURA YA 13

a Mt 24:15-20
Lu 21:20-23

b Lu 21:23
Lu 23:28

c Ufu 7:14

d Da 12:1
Mt 24:21

e Mt 24:22

f Mt 24:23, 24
Lu 17:23
Lu 21:8
1Yo 4:1

g Mt 7:15

h Mt 24:42
Efe 6:18
2Pe 3:17

i Mt 24:29
Lu 21:25, 26

Safu ya 2

a Da 7:13

b Mt 24:30
Lu 21:27
Ufu 1:7

c Mt 24:31

d Mt 24:32
Lu 21:29-33

e Mt 24:33

f Mt 24:34
Lu 21:32

g Isa 51:6

h Yos 23:14
Isa 40:8
Mt 24:35

i Mt 24:36
Mdo 1:7

j Ro 13:11
1Th 5:6

k Mt 25:13
Lu 21:34

l Mt 25:14

m Lu 12:35, 36

n Mt 24:42

o Lu 21:36

lizo katika mbingu zitatikiswa. **26** Ndipo watakapomwona Mwana wa binadamu^a akija katika mawingu akiwa na nguvu nyingi na utukufu.^b **27** Kisha atawatuma malaika wawakusanye watu wake waliochaguliwa kutoka kwenye zile pepo nne, kuanzia mwisho wa dunia mpaka mwisho wa mbingu.^c

28 "Basi jifunzeni mfano huu kutokana na mtini: Mara tu matawi yake machanga yanapokuwa laini na kuchipua majani, mnajua kwamba kiangazi kinakaribia.^d **29** Vivyo hivyo, ninyi pia mtakapoonamambo hayo yakitukia, jueni kwamba yuko karibu, yuko mlangoni.^e **30** Kwa kweli ninawaambia kizazi hiki hakitapitilia mbali kamwe mpaka mambo haya yote yatumie.^f **31** Mbingu na dunia zitapitilia mbali,^g lakini maneno yangu hayatapitilia mbali kamwe.^h

32 "Kuhusu siku hiyo au saa hiyo hakuna mtu anayejua, wala malaika mbinguni wala Mwana, ila Baba.ⁱ **33** Endeeleni kutazama, endeeleni kukaamacho,^j kwa maana hamjui wakati uliowekwa ni lini.^k **34** Ni kama mtu anayesafiri ng'ambo ambaye aliacha nyumba yake na kuwapa watumwa wake mamlaka,^l kila mmoja kazi yake, na kumwamuru mlinzi wa mlango aendelee kukesha.^m **35** Kwa hiyo, endeeleni kukesha, kwa maana hamjui bwana wa nyumba anakuja wakati gani,ⁿ iwe ni jioni, usiku wa manane, kabla ya alfajiri,^{*} au asubuhi na mapema,^o

36 ili anapofika ghafla, asiwakute mkiwa mmelala usingizi.^a 37 Lakini ninachowaaambia ninyi, ninawaambia pia watu wote: Endeeleni kuke-sha.”^b

14 Sasa ilikuwa siku mbi-li kabla^c ya Pasaka^d na Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu.^e Nao wakuu wa makuhani na waandishi walikuwa wakitafuta njia ya kumkamata Yesu kwa hila* na kumuua;^f 2 kwa maana walikuwa wakisema: “Si kwenye sherehe; huenda watu wakafanya ghasia.”

3 Alipokuwa Bethania akila* katika nyumba ya Simoni mwenye ukoma, mwanamke fulani akaja na chupa ya alabasta iliyokuwa na mafuta yenye marashi, nardo halisi, ghali sana. Akaifungua na kuanza kuyamimina juu ya kichwa cha Yesu.^g 4 Ndipo baadhi yao wakakasirika na kuambiana: “Kwa nini mafuta haya ya marashi yapotezwe bure? 5 Kwa maana mafuta haya yangeuzwa kwa zaidi ya dinari* 300 na maskini wapewe pesa hizo!” Nao wakamkasirikia* sana mwanamke huyo. 6 Lakini Yesu akawaambia: “Mwacheni. Kwa nini mnataka kumsumbua? Amenitenda jambo jema.^h 7 Kwa maana maskini mnao sikuzote,ⁱ na mnaweza kuwasaidia wakati wowote mnaotaka, lakini mimi hamtakuwa nami sikuzote.^j 8 Amefanya alichoweza; ameupaka mwili wangu mafuta yenye marashi ili kuutayarisha kwa ajili ya mazi-

14:1 *Au “kwa ujanja.” 14:3 *Au “akiva ameketi mezani.” 14:5 *Angalia Nyongeza B14. ^aAu “wakamkemea.”

SURA YA 13

a Mt 25:5

b Hab 2:3

SURA YA 14

c Yoh 13:1

d Kut 12:3, 6
Law 23:5

e Law 23:6

f Mt 26:2-5
Lu 22:1, 2

g Mt 26:6-9
Yoh 12:2-5

h Mt 26:10
Yoh 12:7

i Kum 15:11

j Mt 26:11
Yoh 12:8

Safu ya 2

a Mt 26:12
Yoh 12:7

b Mt 24:14

c Mt 26:13

d Mt 26:14-16
Lu 22:3-6

e Zek 11:12

f Kut 12:15, 18
Kut 23:15

g Lu 22:1, 7

h Hes 9:2
Mt 26:17-19

i Lu 22:10-13

j Mt 26:20
Lu 22:14

k Zb 41:9
Mt 26:21, 22
Lu 22:21, 23
Yoh 13:21, 22

shi.^a 9 Kwa kweli ninawaambia, popote ambapo habari njema itahubiriwa ulimwenguni,^b jambo alilofanya mwanamke huyu litatajwa ili kumkumbuka.”^c

10 Yuda Iskariote, mmoja wa wale 12, akaenda kwa wakuu wa makuhani ili amsaliti kwao.^d 11 Waliposikia hilo, wakafurahi na kuahidi kumpa fedha.^e Basi akaanza kutafuta nafasi ya kumsaliti.

12 Sasa siku ya kwanza ya Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu,^f wakati ambapo walikuwa na desturi ya kutoa dhabihu ya Pasaka,^g wanafunzi wake wakamwuliza: “Unataka twende tukutayari-shie wapi mlo wa Pasaka?”^h

13 Ndipo akawatuma wawili kati ya wanafunzi wake akawaambia: “Nendeni jijini, nanyi mtakutana na mwanamume akiwa amebeba mtungi wa maji. Mfuatoni,ⁱ 14 na popote atakapoingia, mwambieni mwenye nyumba, ‘Mwalimu anasema: “Kiko wapi chumba cha wageni ambamo ninaweza kula Pasaka pamoja na wanafunzi wangu?”’ 15 Naye atawaonyesha chumba kikubwa cha juu, chenye vifaa na kilichotayarishwa. Tuandalieni humo.” 16 Basi wanafunzi wakaenda, wakaingia jijini na kupata kama alivyowaambia, nao wakaandaa Pasaka.

17 Ilipofika jioni akaja pamoja na wale 12.^j 18 Walipokuwa wameketi mezani wakila, Yesu akasema: “Kwa kweli ninawaambia, mmoja wenu anayekula pamoja nami atanisaliti.”^k 19 Wakaanza kuhuzunika na kumuuliza mmoja baada ya mwingine: “Je, ni

mimi?" **20** Akawaambia: "Ni mmoja kati yenu 12, anayechovya pamoja nami katika bakuli.^a **21** Kwa maana Mwana wa binadamu anaenda zake, kama ilivyoandikwa kumhusu, lakini ole wake mtu atakayemsaliti Mwana wa binadamu!^b Ingekuwa afadhali kama mtu huyo hangezaliwa."^c

22 Walipokuwa wakiendelea kula, akachukua mkaate, akatoa baraka, akaumeza, akawapa, na kusema: "Chukueni; huu unamaanisha mwili wangu."^d **23** Kisha akachukua kikombe, akashukuru na kuwapa, wote wakanywa kutoka kwenye kikombe hicho.^e **24** Akawaambia: "Hii inamaanisha 'damu^f yangu ya agano,^g ambayo itamwagwa kwa ajili ya wengi.^h **25** Kwa kweli ninawaambia, sitakunywa tena kamwe divai ya mzabibu mpaka siku nitakapokunywa ikiwa mpya katika Ufalme wa Mungu." **26** Mwishowe, baada ya kuimba sifa, * wakaenda kwenye Mlima wa Mizeituni.ⁱ

27 Yesu akawaambia: "Ninyi nyote mtakwazika, kwa maana imeandikwa: 'Nitampiga mchungaji,^j nao kondoo watatawanyika.'^k **28** Lakini baada ya kufufuliwa, nitawatangulia kuingia Galilaya."^l **29** Lakini Petro akamwambia: "Hata wengine wote wakikwazika, mimi sitakwazika."^m **30** Ndipo Yesu akamwambia: "Kwa kweli ninakuambia kwamba leo, ndiyo, usiku huu, kabla jogoo hawajika mara mbili, utanikana mara tatu."ⁿ **31** Lakini akae-

14:26 *Au "zaburi."

SURA YA 14

a Mt 26:23

b Lu 22:22

c Mt 26:24

d Mt 26:26
Lu 22:19
1Ko 11:23, 24

e Mt 26:27
1Ko 10:16
1Ko 11:25

f Kut 24:8
Law 17:11
Ebr 9:22

g Yer 31:31
Ebr 7:22
Ebr 9:15

h Isa 53:12
Mt 26:28
Lu 22:20

i Mt 26:30
Lu 22:39
Yoh 18:1

j Isa 53:5
Da 9:26

k Zek 13:7
Mt 26:31-33
Mt 26:56
Mk 14:50
Yoh 16:32

l Mk 16:7

m Lu 22:31-33
Yoh 13:37

n Mt 26:34
Lu 22:34
Yoh 13:38

Safu ya 2

a Mt 26:35

b Mt 26:36, 37
Lu 22:39-41
Yoh 18:1

c Mk 9:2

d Yoh 12:27

e Mt 26:38

f Ro 8:15
Gal 4:6

g Mt 26:39
Lu 22:42
Yoh 6:38
Ebr 5:7

h Mt 26:40
Lu 22:45

i Mt 6:13
Lu 11:4
Lu 22:46

j Mt 26:41
Ro 7:23

k Mt 26:42-46

ndelea kusisitiza: "Hata niki-lazimika kufa pamoja nawe, sitakukana kamwe." Pia, wengine wote wakaanza kusema vivyo hivyo.^a

32 Basi wakafika mahali panapoitwa Gethsemane, akawaambia wanafunzi wake: "Ketini hapa ninaposali."^b

33 Akaondoka pamoja na Petro, Yakobo, na Yohana,^c naye akaanza kufadhaika* na kutaabika sana. **34** Akawaambia: "Nimehuzunika* sana,^d kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mwendelee kukesha."^e

35 Akasonga mbele kidogo, akaanguka chini na kuanza kusali kwamba ikiwezekana, saa hiyo ipitilie mbali kutoka kwake. **36** Naye akasema: "Abba,* Baba,^f mambo yote yanawezekana kwako; niondolee kikombe hiki. Lakini si kama ninavyotaka, bali unavyotaka."^g **37** Aliporudi akawakuta wakijiwa wamelala usingizi, akamwuliza Petro: "Simoni, unalala? Hukuwa na nguvu za kukesha hata kwa saa moja?"^h **38** Endelee ni kukesha na kusali bila kucha, ili msingie katika majaribu.ⁱ Bila shaka, roho inataka,* lakini mwili ni dhaifu."^j

39 Naye akaenda zake tena, akasali, akirudia maneno yaleyale.^k **40** Akaja tena na kuwakuta wakiwa wamelala usingizi, kwa maana macho yao yalikuwa yamelemewa, nao hawakujua la kumjibu. **41** Akarudi mara ya tatu akawaambia: "Mnalala na kupumzika wakati

14:33 *Au "kuhisi mshtuko." 14:34

*Au "Nafsi yangu imehuzunika." 14:36

*Neno la Kiebrania au Kiaramu linalo-manisha "Ee Baba!" 14:38 *Au "inapenda."

kama huu! Imetosh! Saa imefika!^a Tazama! Mwana wa binadamu anasalitiwa mikononi mwa watenda dhambi. **42** Simameni twende. Tazama! Msaliti wangu amekaribia.”^b

43 Na mara moja, alipokuwa bado akizungumza, Yuda, mmoja wa wale 12, akafika pamoja na umati wenye mapanga na marungu, walikuwa wametumwa na wakuu wa makuhani, waandishi, na wazee.^c **44** Basi msaliti wake alikuwa amewapa ishara waliyokubaliana akisema: “Yule nita-kayembusu, huyo ndiye; mkamateni na kuondoka naye akiwa chini ya ulinzi.” **45** Akaja moja kwa moja akamkaribia na kusema, “Rabi!” kisha akambusu kwa wororo. **46** Basi wakamkamata na kumtia nguvuni. **47** Hata hivyo, mmoja wa wale waliokuwa wamesimama hapo akauchomoa upanga wake, akampiga mtumwa wa kuhani mkuu na kumkata sikio.^d **48** Lakini Yesu akawaambia: “Je, mmekuja kuni-kamata mkiwa na mapanga na marungu kana kwamba mimi ni mwizi?”^e **49** Siku baada ya siku nilikuwa nanyi nikifundisha hekaluni,^f lakini hamkunikamata. Hata hivyo, ni ili Maandiko yatimizwe.”^g

50 Ndipo wote wakamwachana na kukimbia.^h **51** Hata hivyo, kijana fulani aliyevaa vazi la kitani bora juu ya mwili wake ulio uchi akaanza kumfuata kwa karibu, nao wakaribu kumkamata, **52** lakini akaliacha vazi lake la kitani, akakimbia akiwa uchi.*

14:52 *Au “akiwa amevaa mavazi machache; akiwa na vazi la ndani tu.”

SURA YA 14

a Yoh 13:1

b Yoh 18:2

c Mt 26:47-51

Lu 22:47-51

Yoh 18:3

d Mt 26:51

Lu 22:50

Yoh 18:10

e Mt 26:55, 56

Lu 22:52, 53

f Lu 19:47

Yoh 18:20

g Zb 22:6

Isa 53:7

Da 9:26

Lu 22:37

h Zek 13:7

Mt 26:31

Yoh 16:32

Safu ya 2

a Yoh 18:13

b Mt 26:57

Lu 22:54, 55

c Mt 26:58

Yoh 18:15

d Mt 26:59, 60

e Zb 35:11

f Mt 26:61

Mk 15:29

Yoh 2:19

g Mt 26:62, 63

h Isa 53:7

1Pe 2:23

i Da 7:13

j Zb 110:1

Efe 1:20

Kol 3:1

k Mt 24:30

Mt 26:64

Lu 21:27

Ufu 1:7

l Mt 26:65, 66

53 Kisha wakampeleka Yesu kwa kuhani mkuu,^a nao wakuu wote wa makuhani, wazee, na waandishi wakakusanyika.^b **54** Lakini Petro akamfuata kwa mbali mpaka kwenye ua wa kuhani mkuu; akaketi pamoja na watumishi wa nyumbani akiota moto mwangavu.^c **55** Sasa wakuu wa makuhani na Sanhedrini yote walikuwa wakitafuta ushahidi dhidi ya Yesu ili wamuue, lakini hawakupata.^d **56** Kwa kweli, wengi walikuwa wakitoa ushahidi wa uwongo kumhusu,^e lakini ushahidi wao haukupatana. **57** Pia, wengine walikuwa wakisimama na kutoa ushahidi wa uwongo kumhusu, wakisema: **58** “Tulimsikia akisema, ‘Nitaliangusha chini hekalu hili lililojengwa kwa mikono, na kwa siku tatu nitajenga lingine ambalo halijajengwa kwa mikono.’”^f **59** Lakini hata kwa misingi hiyo, ushahidi wao haukupatana.

60 Kisha kuhani mkuu akasimama katikati yao, akamuuliza Yesu: “Kwa nini hujibu? Watu hawa wanashuhudia nini kukuhusu?”^g **61** Lakini akakaa kimya na hakujibu.^h Tena kuhani mkuu akaanza kumuuliza: “Je, wewe ndiye Kristo Mwana wa Yule Mbarikiwa?” **62** Ndipo Yesu akasema: “Mimi ndiye; nanyi mtamwona Mwana wa binadamu/ akiwa ameketi kwenye mkono wa kuume/ wa nguvu, akija pamoja na mawingu ya mbinguni.”^k **63** Ndipo kuhani mkuu akayarara mavazi yake na kusema: “Tunahitaji mashahidi wengine wa nini?”^l **64** Mmemsikia akikufuru. Uamuzi

wenu ni nini?*" Wote wakaamua kwamba anastahili kufa.^a **65** Wengine wakaanza kumtemea mate,^b wakamfunika uso, wakampiga ngumi na kumwambia: "Toa unabii!" Walinzi wa mahakama wakampiga makofi usoni na kumchukua.^c

66 Sasa Petro alipokuwa chini katika ua, mmoja wa wajakazi wa kuhani mkuu akaja.^d **67** Alipomwona Petro akiota moto, akamtazama moja kwa moja na kusema: "Hata wewe ulikuwa pamoja na Yesu Mnazareti." **68** Lakini akakana, akisema: "Simjui wala sielewi unachosema." Kisha akatoka na kuelekea langoni.* **69** Yule kijakazi alipomwona akaanza tena kuwaambia wale waliosimama hapo: "Huyu ni mmoja wao." **70** Petro akakana tena. Bada ya muda mfupi, wale waliosimama hapo wakaanza tena kumwambia: "Hakika wewe ni mmoja wao, kwa maana, wewe ni Mgalilaya." **71** Lakini akaanza kulaani na kuapa: "Simjui mtu huyu mnayezungumza kumhusu!" **72** Papo hapo jogoo akawika mara ya pili,^e naye Petro akakumbuka maneno ambayo Yesu alimwambia: "Kabla jogoo hawawika mara mbili, utanikana mara tatu."^f Naye akalemewa akaanza kulia.

15 Mara tu kulipopambazuka wakuu wa makuhani, wazee, na waandishi, yaani, Sanhedrini yote, wakashauriana pamoja na kumfunga Yesu, kisha wakampeleka na kumkabidhi kwa Pila-

14:64 *Au "Mnaonaje?" 14:68 *Au "sebuleni."

SURA YA 14

a Law 24:16
Yoh 19:7

b Isa 50:6
Isa 53:3
Mt 26:67, 68

c Lu 22:63-65

d Mt 26:69-75
Lu 22:55-62
Yoh 18:25, 26

e Yoh 18:27

f Mt 26:34
Mk 14:30
Lu 22:34
Yoh 13:38

Safu ya 2

SURA YA 15

a Zb 2:2
Mt 27:1, 2
Lu 22:66
Yoh 18:28
Mdo 3:13
Mdo 4:26

b Yoh 18:33, 37

c Mt 27:11-14
Lu 23:3

d Mt 26:62

e Yoh 19:9, 10

f Isa 53:7

g Mt 27:15-18
Yoh 18:39

h Lu 23:16

i Mt 21:38

j Mt 27:20-23
Mdo 3:14

k Lu 23:20-25

l Yoh 19:6

m Mdo 3:13
Mdo 13:28

to.^a **2** Basi Pilato akamuuliza: "Je, wewe ndiye Mfalme wa Wayahudi?"^b Akamjibu: "Wewe mwenyewe umesema."^c **3** Lakini wakuu wa makuhani walikuwa wakimshtaki kwa mambo mengi. **4** Pilato akaanza kumuuliza tena: "Je, huna jibu lolote?"^d Ona ni mashtaka mangapi wanaoleta dhidi yako."^e **5** Lakini Yesu hakujibu tena, hivi kwamba Pilato akashangaa.^f

6 Basi, kila sherehe ya Pasaka, alikuwa na desturi ya kuwafungulia mfungwa ambaye waliomba.^g **7** Wakati huo mtu aliyetitwa Baraba alikuwa amefungwa pamoja na wachochezi ambao katika uchochezi wao walikuwa wameua. **8** Basi umati ukaja na kuanza kumwomba Pilato awafanyie kama ilivyokuwa desturi yake. **9** Akawauliza: "Je, mnataka niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?"^h **10** Kwa maana Pilato alijua kwamba wakuu wa makuhani walikuwa wamemkabidhi Yesu kwake kwa sababu ya wivu.ⁱ **11** Lakini wakuu wa makuhani wakaichochea umati umwombe awafungulie Baraba badala yake.^j **12** Pilato akawauliza tena: "Basi, nifanye nini na mtu huyu mnayemwita Mfalme wa Wayahudi?"^k **13** Kwa mara nyingine tena wakapaza sauti: "Atundikwe mtni!"^l **14** Lakini Pilato akawaambia: "Kwa nini? Amefanya kosa gani?" Hata hivyo, wakaendelea kupaza sauti hata zaidi: "Atundikwe mtni!"^m **15** Basi Pilato akitaka kuuridhisha umati, akawafungulia Baraba; akaagi-

15:13, 14 *Au "Auawe kwenye mtni!"

za Yesu apigwe mijeledi,^a kisha akamtoa ili auawe kwenye mti.^b

16 Sasa wanajeshi wakampeleka kwenye ua, katika makao ya gavana, nao wakakusanya kikosi chote cha wanajeshi.^c **17** Wakamvika Yesu vazi la zambarau, wakasokota taji la miiba na kumvisha; **18** nao wakaanza kumwambia kwa sauti kubwa: "Salamu,* ewe Mfalme wa Wayahudi!"^d **19** Pia, walikuwa wakimpiga kichwani kwa utete na kumtemea mate, nao wakapiga magoti na kumsujudia.* **20** Mwishowe, baada ya kumdhahaki, wakamvua lile vazi la zambarau na kumvisha mavazi yake ya nje. Kisha wakampeleka ili kumtundika mtini.^e **21** Pia, wakamlazimisha mpita njia afanye utumishi, mtu fulani aitwaye Simoni wa Kirene, baba ya Aleksanda na Rufo, aliyekuwa akitoka mashambani, aubebe mti wa mateso* wa Yesu.^f

22 Basi wakampeleka mahali panapoitwa *Golgotha*, neno ambalo linapotafsiriwa linamaanisha, "Mahali pa Fuvu la Kichwa."^g **23** Hapa wakajaribu kumpa divai iliyotiwa kileo cha manemane,^h lakini hakuniywa. **24** Nao wakamtundika kwenye mti na wakagawana mavazi yake kwa kuyapigia kura ili kuamua ni nini ambacho kila mtu angechukua.ⁱ **25** Ilikuwa saa tatu,* nao wakamtundika kwenye mti. **26** Na maandishi ya mashta-

15:18 *Au "Usifiwe." 15:19 *Au "kumwinamia." 15:21, 30, 32 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 15:25 *Yaani, karibu saa tatu asubuhi.

SURA YA 15

a Yoh 19:1

b Mt 27:24, 26

c Mt 27:27-31

d Yoh 19:3

e Yoh 19:16

f Mt 27:32
Lu 23:26g Mt 27:33-37
Lu 23:33
Yoh 19:17
Ebr 13:12

h Zb 69:21

i Zb 22:18
Yoh 19:23, 24

Safu ya 2

a Mt 27:29, 37
Lu 23:38
Yoh 19:19

b Mt 27:38

c Zb 22:7
Zb 109:25
Isa 53:3d Mt 27:39-42
Mk 14:58

e Lu 23:35

f Mt 16:4

g Mt 27:44
1Pe 2:23h Mt 27:45
Lu 23:44i Zb 22:1
Mt 27:46-49j Zb 69:21
Yoh 19:29

ka dhidi yake yalikuwa yameandikwa: "Mfalme wa Wayahudi."^a **27** Pia, wakawatundika wezi wawili kwenye mti kando yake, mmoja upande wake wa kuume na mwingine upande wake wa kushoto.^b **28** *— **29** Wale waliokuwa wakipita hapo wakamtukana huku wakitikisa vichwa vyao^c wakisema: "Aha! Wewe uliyetaka ku-liangusha chini hekalu na kulijenga kwa siku tatu,^d **30** jio koe mwenyewe kwa kushuka kutoka kwenye mti wa mateso."^e **31** Vivyo hivyo, wakuu wa makuhani na waandishi walikuwa wakimdhahaki kati yao wakisema: "Aliwaokoa wengine lakini hawezi kujiokoa mwenyewe!"^e **32** Acheni Kristo, Mfalme wa Israeli, ashuke sasa kutoka kwenye mti wa mateso,* ili tuone na kuamini.^f Hata wale waliotundikwa mtini kando yake walikuwa wakimshutumua.^g

33 Ilipofika saa sita* kuka-wa na giza katika nchi yote mpaka saa tisa.^h **34** Na saa tisa Yesu akapaza sauti: "*Eli, Eli, lama sabakhani?*" maneno hayo yanapotafsiriwa yanamaanisha, "Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini ume-niacha?"ⁱ **35** Na baadhi ya wale waliokuwa wamesimama karibu walipomsikia wakaaanza kusema: "Sikia! Anamwita Eliya." **36** Kisha mtu fulani akakimbia, akalowesha sifongo katika divai kali, akaiweka kwenye utete, akampa anywe,^j akisema: "Mwacheni! Acheni tuone kama Eliya atakuja kumshusha." **37** Lakini

15:28 *Angalia Nyongeza A3. 15:33 *Yaani, karibu saa 6 mchana. ^aYaani, karibu saa 9 alasiri.

Yesu akalia kwa sauti kubwa, akakata pumzi.*^a **38** Na pazia la patakatifu^b likapasuka vipande viwili kuanzia juu mpaka chini.^c **39** Sasa ofisa wa jeshi aliyekuwa amesimama kando yake akimtazama, alipoona amekufa katika hali hizo, akasema: “Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu.”^d

40 Kulikuwa pia na wanawake wakitazama kwa mbali, miongoni mwao kulikuwa na Maria Magdalene, Salome, na Maria mama ya Yakobo Mdogo na Yose,^e **41** walikuwa waki-fuatana na Yesu na kumhudumia^f alipokuwa Galilaya, pia wanawake wengine wengi waliokuwa wamekuja Yerusalemu pamoja naye.

42 Sasa kwa kuwa ilikuwa jioni, siku ya Matayarisho, yaani, siku moja kabla ya Sabato, **43** akaja Yosefu wa Arimathea, mshiriki wa Baraza aliyeheshimiwa, ambaye pia alikuwa akiungojea Ufalme wa Mungu. Akajipa moyo na kwenda kwa Pilato, akaoomba apewe mwili wa Yesu.^g **44** Lakini Pilato akataka kujua kama tayari alikuwa amekufa, akamwita yule ofisa wa jeshi, akamuuliza ikiwa Yesu alikuwa amekufa. **45** Baada ya kuhakikisha kutoka kwa huyo ofisa wa jeshi, akamruhusu Yosefu auchukue mwili huo. **46** Baada ya kununua kitani bora, akamshusha na kumfunga kwa kile kitani bora na kumlaza katika kaburi*^h lililokuwa limechimbwa katika mwamba; ki-

15:37 *Au “akapumua mara ya mwisho.”
15:46 *Au “kaburi la ukumbusho.”

SURA YA 15

a Zb 31:5
Mt 27:50
Lu 23:46
Yoh 19:30

b Kut 26:31-33
Ebr 6:19

c Mt 27:51
Lu 23:45
Ebr 10:19, 20

d Mt 27:54
Lu 23:47

e Mt 27:55, 56
Lu 23:49

f Lu 8:2, 3

g Kum 21:22, 23
Mt 27:57, 58
Lu 23:50-52
Yoh 19:38

h Isa 53:9

Safu ya 2

a Mt 27:59, 60
Lu 23:53
Yoh 19:40

b Mt 27:61
Lu 23:55

SURA YA 16

c Kut 20:8, 9

d Mt 28:1

e Lu 23:55, 56

f Lu 24:1
Yoh 20:1

g Lu 24:2, 3

h Lu 24:4

i Mk 8:31
Lu 18:33
Mdo 4:10

j Mt 28:5, 6

k Mt 26:32
Mk 14:28

l Mt 28:7

m Mt 28:8
Lu 24:9

sha akaviringisha jiwe kwenye mwingilio wa lile kaburi.^a **47** Lakini Maria Magdalene na Maria mama ya Yose wakaendelea kutazama mahali alipokuwa amelazwa.^b

16 Baada ya Sabato^c kupita, Maria Magdalene, Maria^d mama ya Yakobo, na Salome wakanunua manukato ili wakaupake mwili wa Yesu.^e **2** Asubuhi na mapema siku ya kwanza ya juma, jua lilipokuwa limechomoza, wakaenda kwenye kaburi.*^f **3** Walikuwa wakiulizana: “Ni nani atakayetuviringishia lile jiwe kutoka kwenye mwingilio wa kaburi?” **4** Lakini walipotazama, wakaona lile jiwe lilikuwa limeondolewa, ingawa lilikuwa kubwa sana.^g **5** Walipoiingia ndani ya kaburi, wakaona mwanamume kijana akiwa ameketi upande wa kulia akiwa amevaa kanzu nyeupe, nao wakashuka. **6** Akawaambia: “Msishtuke.^h Mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyeeua kwenye mti. Amefufuliwa.ⁱ Hayupo hapa. Tazama, hapa ndipo walipomlaza.^j **7** Lakini nendeni mkawaambie wanafunzi wake na Petro, ‘Yesu anawatangulia kwenda Galilaya.^k Mtamwona huko, kama vile alivyowaambia.’”^l **8** Basi walipotoka kaburini, wakakimbia wakitetemeka huku wakiwa wamelemewa na hisia. Nao hawakumwambia mtu yeyote jambo lolote, kwa sababu waliogopa.*^m

16:2 *Au “kwenye kaburi la ukumbusho.”
16:8 *Kulingana na hati za kale zinazotegemeka, Injili ya Marko inafikia mwisho kwa maneno yaliyo kwenye mstari wa 8. Angalia Nyongeza A3.

YALIYOMO

- 1 Ujumbe kwa Theofilo (1-4)
Gabrieli atabiri kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji (5-25)
Gabrieli atabiri kuzaliwa kwa Yesu (26-38)
Maria amtembelea Elisabeti (39-45)
Maria amtukuza Yehova (46-56)
Yohana azaliwa na kupewa jina (57-66)
Unabii wa Zekaria (67-80)
- 2 Yesu azaliwa (1-7)
Malaika wawatokea wachungaji (8-20)
Tohara na kutakaswa (21-24)
Simeoni amwona Kristo (25-35)
Ana azungumza kumhusu mtoto (36-38)
Warudi Nazareti (39, 40)
Yesu aenda hekaluni akiwa na miaka 12 (41-52)
- 3 Yohana aanza kazi yake (1, 2)
Yohana ahubiri kuhusu ubatizo (3-20)
Yesu abatizwa (21, 22)
Ukoo wa Yesu Kristo (23-38)
- 4 Ibilisi amjaribu Yesu (1-13)
Yesu aanza kuhubiri huko Galilaya (14, 15)
Yesu akataliwa huko Nazareti (16-30)
Yesu akiwa katika sinagogi huko Kapernaumu (31-37)
Mama mkwe wa Simoni na wagonjwa wengine waponywa (38-41)
Umati wampata Yesu katika eneo lisilo na watu (42-44)
- 5 Wavua samaki kimuujiza; wanafunzi wa kwanza (1-11)
Mtu mwenye ukoma aponywa (12-16)
Yesu amponya mtu aliyepooza (17-26)
Yesu amwita Lawi (27-32)
Swali kuhusu kufunga (33-39)
- 6 Yesu ndiye "Bwana wa Sabato" (1-5)
Mtu aliyepooza mkono aponywa (6-11)
Mitume 12 (12-16)
Yesu afundisha na kuponya (17-19)
Furaha na ole (20-26)
Kuwapenda adui (27-36)
Acheni kuhukumu (37-42)
- Mti hujulikana kwa matunda yake (43-45)
Nyumba iliyojengwa vizuri; nyumba isiyo na msingi imara (46-49)
- 7 Ofisa wa jeshi mwenye imani (1-10)
Yesu amfufua mwana wa mjane huko Naini (11-17)
Yohana Mbatizaji asifiwa (18-30)
Kizazi kisicho na imani chashutumwiwa (31-35)
Mwanamke mwenye dhambi asamehewa (36-50)
Mfano wa watu wenye madeni (41-43)
- 8 Wanawake waliomfuata Yesu (1-3)
Mfano wa mpandaji (4-8)
Kwa nini Yesu alitumia mifano? (9, 10)
Mfano wa mpandaji wafafanuliwa (11-15)
Taa haipaswi kufunikwa (16-18)
Mama na ndugu za Yesu (19-21)
Yesu atuliza dhoruba (22-25)
Yesu awaruhusu roho waovu waingie ndani ya nguruwe (26-39)
Binti ya Yairo; mwanamke agusa mavazi ya nje ya Yesu (40-56)
- 9 Wale 12 wapewa maagizo kuhusu huduma (1-6)
Herode ahangazwa na Yesu (7-9)
Yesu awalisha wanaume 5,000 (10-17)
Petro amtambua Kristo (18-20)
Kifo cha Yesu chatabiriwa (21, 22)
Wanafunzi wa kweli (23-27)
Yesu ageuka sura (28-36)
Mvulana aliyekuwa na roho mwovu aponywa (37-43a)
Kifo cha Yesu chatabiriwa tena (43b-45)
Wanafunzi wabishana kuhusu cheo (46-48)
Asiyetupinga yuko upande wetu (49, 50)
Kijiji cha Wasamaria chamkataa Yesu (51-56)
Jinsi ya kumfuata Yesu (57-62)
- 10 Yesu awatuma wale 70 (1-12)
Ole kwa miji isiyotubu (13-16)
Wale 70 warudi (17-20)

- Yesu amsifu Baba yake
kwa kuwafunulia mambo
wanyenyekevu (21-24)
Mfano wa Msamaria mwema (25-37)
Yesu awatembelea Martha na
Maria (38-42)
- 11 Jinsi ya kusali (1-13)
Sala ya mfano (2-4)
Roho waovu wafukuzwa kwa
nguvu za Mungu (14-23)
Roho mwovu arudi (24-26)
Furaha ya kweli (27, 28)
Ishara ya Yona (29-32)
Taa ya mwili (33-36)
Ole kwa wanafiki wa kidini (37-54)
- 12 Chachu ya Mafarisayo (1-3)
Mwogope Mungu, si wanadamu (4-7)
Kukiri muungano na Kristo (8-12)
Mfano wa tajiri mpumbavu (13-21)
Acheni kuhangaika (22-34)
Kundi dogo (32)
Kukeshwa (35-40)
Msimamizi mwaminifu na msimamizi
asiye mwaminifu (41-48)
Si amani, bali mgawanyiko (49-53)
Uhitaji wa kuchunguza nyakati (54-56)
Kutatua mizozo (57-59)
- 13 Tubuni au muangamizwe (1-5)
Mfano wa mtini usiozaa (6-9)
Mwanamke mlemavu aponywa siku ya
Sabato (10-17)
Mfano wa mbegu ya haradali na wa
chachu (18-21)
Jitihada zinahitajika ili kupitia mlango
mwembamba (22-30)
Herode, "mbweha huyo" (31-33)
Yesu aombolezea Yerusalemu (34, 35)
- 14 Mtu mwenye ugonjwa wa kuvimba
aponywa siku ya Sabato (1-6)
Uwe mgeni mnyenyekevu (7-11)
Waalike watu wasio na uwezo wa
kukulipa (12-14)
Mfano wa wageni waliotoa
visingizio (15-24)
Gharama ya kuwa mwanafunzi (25-33)
Chumvi inapoteza nguvu yake (34, 35)
- 15 Mfano wa kondoo aliyepotea (1-7)
Mfano wa sarafu iliyopotea (8-10)
Mfano wa mwana mpotevu (11-32)
- 16 Mfano wa msimamizi asiye
mwadilifu (1-13)
'Mtu mwaminifu katika dogo ni
mwaminifu katika kubwa' (10)
Sheria na Ufalme wa Mungu (14-18)
Mfano wa tajiri na Lazaro (19-31)
- 17 Kukwazika, msamaha, na imani (1-6)
Watumwa wasiofaa kitu (7-10)
Watu kumi wenye ukoma
waponywa (11-19)
Kuja kwa Ufalme wa Mungu (20-37)
"Ufalme wa Mungu uko katikati
yenu." (21)
"Mkumbukeni mke wa Loti" (32)
- 18 Mfano wa mjane aliyeendelea
kuomba (1-8)
Farisayo na mkusanya kodi (9-14)
Yesu na watoto (15-17)
Mtawala tajiri auliza swali (18-30)
Kifo cha Yesu chatabiriwa tena (31-34)
Kipofu aliyekuwa akiombaomba
aponywa (35-43)
- 19 Yesu amtembelea Zakayo (1-10)
Mfano wa mina kumi (11-27)
Yesu aingia kwa kishindo (28-40)
Yesu alililia jiji la Yerusalemu (41-44)
Yesu asafisha hekalu (45-48)
- 20 Wataka kujua chanzo cha mamlaka
ya Yesu (1-8)
Mfano wa wakulima wauaji (9-19)
Mungu na Kaisari (20-26)
Swali kuhusu ufufuo (27-40)
Je, Kristo ni mwana wa Daudi? (41-44)
Onyo dhidi ya waandishi (45-47)
- 21 Sarafu mbili za mjane maskini (1-4)
ISHARA YA MAMBO YATAKAYOKUJA (5-36)
Vita, matetemeko makubwa ya
ardhi, magonjwa, upungufu wa
chakula (10, 11)
Yerusalemu lazingerwa na
majeshi (20)
Nyakati zilizowekwa za mataifa (24)
Kuja kwa Mwana wa binadamu (27)
Mfano wa mtini (29-33)
Endeleeni kukeshwa (34-36)
Yesu afundisha hekaluni (37, 38)
- 22 Makuhani wapanga njama ya kumuua
Yesu (1-6)

Matayarisho ya Pasaka ya mwisho (7-13)

Mlo wa Jioni wa Bwana

waanzishwa (14-20)

'Msaliti wangu yuko pamoja nami mezani' (21-23)

Wabishana vikali kuhusu aliye mkuu zaidi (24-27)

Yesu afanya agano kwa ajili ya ufalme (28-30)

Yesu atabiri Petro atamkana (31-34)

Uhitaji wa kuwa tayari; panga mbili (35-38)

Yesu asali kwenye Mlima wa Mizeituni (39-46)

Yesu akamatwa (47-53)

Petro amkana Yesu (54-62)

Yesu adhihakiwa (63-65)

Kesi mbele ya Sanhedrini (66-71)

23 Yesu mbele ya Pilato na Herode (1-25)

Yesu na wahalifu wawili watundikwa kwenye mti (26-43)

"Utakuwa pamoja nami katika Paradiso" (43)

Yesu afa (44-49)

Yesu azikwa (50-56)

24 Yesu afufuliwa (1-12)

Wakiwa njiani kuelekea Emau (13-35)

Yesu awatokea wanafunzi (36-49)

Yesu apaa mbinguni (50-53)

1 Kwa kuwa watu wengi wamejitahidi kukusanya habari kuhusu mambo ambayo tunayasadiki kabisa,^a **2** kama tulivyoyapokea kutoka kwa wale waliokuwa mashahidi wa kujionea tangu mwanzo^b na wahudumu wa ujumbe,^c **3** mheshimiwa Theofilo,^d mimi pia nimefuatilia mambo yote kwa usahihi tangu mwanzo, nami nimeamua kukuandikia mambo hayo kwa utaratibu mzuri, **4** ili ujue kikamili uhakika wa mambo uliyofundishwa kwa mdomo.^e

5 Katika siku za Herode,^{*f} mfalme wa Yudea, kulikuwa na kuhani aliyemitwa Zekaria wa kikundi cha Abiya.^g Mke wake aliitwa Elisabeti na alikuwa wa ukoo wa Haruni. **6** Wote wawili walikuwa waadilifu mbele za Mungu na walitembea bila lawama kulingana na amri na sheria zote za Yehova.* **7** Lakini hawakuwa na mtoto, kwa

1:5 * Angalia Kamusi, uku. 2012. 1:6, 9, 11, 15 * Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 1

a Yoh 20:30, 31

b Yoh 15:27

1Pe 5:1

2Pe 1:16

c Ebr 2:3

d Mdo 1:1

e Yoh 20:30, 31

f Mt 2:1

g 1Nya 24:3, 10

Safu ya 2

a 1Nya 24:1, 19

2Nya 8:14

2Nya 31:2

b Kut 40:5

c Kut 30:7,8

d Lu 1:59,60

e Lu 1:57,58

f Lu 7:28

sababu Elisabeti alikuwa tasa, na wote wawili walikuwa wamezeeka.

8 Alipokuwa akihudumu akiwa kuhani mbele za Mungu wakati wa zamu ya kikundi chake,^a **9** kulingana na desturi ya[#] ukuhani zamu yake ikafika ya kuingia patakatifu pa Yehova*^b ili kufukiza uvumba.^c **10** Umati wote ulikuwa nje ukisali saa hiyo ya kufukiza uvumba. **11** Malaika wa Yehova* akamtokea, akiwa amesimama upande wa kulia wa madhabahu ya uvumba. **12** Lakini Zekaria alihangai-shwa na jambo aliloona, akaogopa sana. **13** Hata hivyo, malaika akamwambia: "Usiogope, Zekaria, kwa sababu dua yako imesikiwa vema, na mke wako Elisabeti atakuzalia mwana, nawe utamwita Yohana.^d **14** Utakuwa na shangwe na furaha nyingi, na wengi watashangilia atakapozaliwa,^e **15** kwa maana atakuwa mkuu mbele za Yehova.*^f Lakini hapaswi kamwe

1:9 [#] Au "zoea la."

kunywa divai wala kileo,^a naye atajazwa roho takatifu hata kabla ya kuzaliwa,^b **16** naye atawarudisha wana wengi wa Israeli kwa Yehova* Mungu wao.^c **17** Pia, atamtangulia kwa roho na nguvu za Eliya,^d ili kurudisha mioyo ya akina baba kwa watoto^e na wale wasiotii kwenye hekima ya waadilifu, na kumwandalia Yehova* watu waliotayarishwa.”^f

18 Zekaria akamuuliza malaika: “Ninawezaje kuwa na uhakika kuhusu jambo hili? Kwa maana nimezeeka, nao umri wa mke wangu pia ume-songa.” **19** Malaika akamjibu: “Mimi ni Gabrieli,^g ninayesimama karibu mbele za Mungu,^h nami nilitumwa nizingumze nawe na kukutangazia habari hii njema. **20** Lakini tazama! utakaa kima, hutaweza kuongea mpaka siku ambayo mambo hayo yatatendeka, kwa sababu hukumani maneno yangu ambayo yatatimizwa katika wakati uliowekwa.” **21** Watu wakaendelea kumsubiri Zekaria, nao wakashangaa kwa sababu alikuwa amekawia sana katika patakatifu. **22** Alipotoka hakuweza kuzungumza nao, basi wakajua kwamba alikuwa ameona jambo la kustaajibisha* katika patakatifu. Akaendelea kuwafanyia ishara lakini hakuweza kuongea. **23** Siku zake za utumishi mtakatifu* zilipokwisha, akarudi nyumbani.

24 Baada ya siku chache Elisabeti mke wake akapata

1:15 *Au “tangu akiwa katika tumbo la mama yake.” 1:16, 17, 25, 28, 32 *Angalia Nyongeza A5. 1:22 *Au “maono.” 1:23 *Au “utumishi wake wa watu wote.”

SURA YA 1

a Hes 6:2, 3
Mt 11:18

b Yer 1:5
Ro 9:10-12

c Mal 4:6

d Mt 11:13, 14
Mt 17:10-12

e Mal 4:5, 6

f Isa 40:3
Mal 3:1

g Da 8:16
Da 9:21
Lu 1:26, 27

h Ebr 1:7, 14

Safu ya 2

a Mwa 30:22, 23
Isa 1:10, 11

b Da 8:16
Lu 1:19

c Isa 7:14

d Mt 1:18

e Gal 4:4

f Mt 1:21-23
Lu 2:21

g Flp 2:9-11
ITI 6:15

h Mt 27:54
Yoh 1:49

i 2Sa 7:8, 12
Zb 132:11
Isa 9:7
Isa 11:1, 10
Yer 23:5
Mt 1:1

j Da 2:44
Da 7:13, 14
Ebr 1:8

k Isa 7:14
Mt 1:24, 25

l Mt 1:18, 20

m Yoh 6:68, 69

n Mt 14:33
Yoh 1:32, 34
Yoh 20:31

mimba, naye hakutoka nyumbani kwa miezi mitano. Alikuwa akisema: **25** “Yehova* amenitendea hivi katika siku hizi. Amenikumbuka ili kuniondolea aibu kati ya watu.”^a

26 Katika mwezi wake wa sita, malaika Gabrieli^b akatumwa na Mungu aende katika jiji la Nazareti huko Galilaya, **27** kwa bikira^c aliyetitwa Maria,^d mchumba wa mwanamume aliyetitwa Yosefu wa nyumba ya Daudi. **28** Malaika akaja na kumwambia: “Salamu, wewe uliyebarikiwa sana, Yehova* yuko pamoja nawe.”

29 Lakini Maria akahangai-shwa sana na maneno aliyoyambiwa, naye aanza kufikiria maana ya salamu hizo.

30 Basi malaika akamwambia: “Usiogope, Maria, kwa maana umepata kibali cha Mungu. **31** Tazama! utapata mimba* na kuzaa mwana^e nawe utamwita Yesu.^f **32** Huyu atakuwa mkuu^g naye ataitwa Mwana wa Aliye Juu Zaidi,^h na Yehova* Mungu atampa kiti cha ufalme cha Daudi baba yake,ⁱ **33** naye atatawala akiwa Mfalme juu ya nyumba ya Yakobo milele, na Ufalme wake hautakuwa na mwisho.”^j

34 Lakini Maria akamuuliza malaika: “Hilo litawezekana naje, kwa kuwa sina uhusiano wa kingono na mwanamume?”^k **35** Malaika akamjibu: “Roho takatifu itakuja juu yako,^l na nguvu za Aliye Juu Zaidi zitakufunika. Kwa hiyo yule atakayezaliwa ataitwa mtakatifu,^m Mwana wa Mungu.ⁿ **36** Tazama! Hata Elisabeti mtu wako wa ukoo,

1:31 *Au “utachukua mimba katika tumbo lako la uzazi.”

ingawa amezeeka ana mimba ya miezi sita, yule anayejulikana kuwa tasa; **37** kwa sababu kwa Mungu haku-na tangazo* lisilowezekana.”^a **38** Ndipo Maria akasema: “Tazama! Kijakazi wa Yehova!* Na itendeke kwangu kulingana na tangazo lako.” Kisha malaika akaondoka.

39 Basi siku hizo, Maria akafunga safari haraka kwenenda kwenye eneo lenye milima, mpaka jiji fulani la Yuda, **40** naye akaingia nyumbani kwa Zekaria na kumsalimu Elisabeti. **41** Elisabeti aliposikia salamu za Maria, mtoto aliyekuwa tumboni mwake akaruka, naye Elisabeti akajazwa roho takatifu **42** na kusema kwa sauti kubwa: “Umebarikiwa kati ya wanawake, na uzao wa tumbo lako umebarikiwa! **43** Imekuwaje nimependelewa hivi kwamba mama ya Bwana wangu amenitembelea? **44** Kwa maana tazama! Niliposikia salamu zako, mtoto aliye tumboni mwangu aliruka kwa shangwe. **45** Mwenye furaha pia ni yule aliyeamini, kwa sababu atatimizwa kikamilimambo aliyambiwa kuto-ka kwa Yehova.”*

46 Naye Maria akasema: “Nafsi” yangu inamtukuzza Yehova,*^b **47** na roho yangu haitaacha kumshangilia Mungu Mwokozi wangu,^c **48** kwa sababu ametazama hali ya chini ya kijakazi wake.^d Tazama! tangu sasa vizazi vyote vitanitangaza kuwa mwenye furaha,^e **49** kwa sababu Mwenye nguvu amenitendea

1:37 *Au “jambo lolote.” 1:38, 45, 46, 58 *Angalia Nyongeza A5. 1:46 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 1

a Mwa 18:14
Mt 19:26

b 1Sa 2:1

c 2Sa 22:3
Isa 43:3
Hab 3:18
Tit 1:3
Yud 25

d 1Sa 1:10,11

e Lu 11:27

Safu ya 2

a Zb 71:19
Zb 111:9

b Zb 103:17

c 2Sa 22:28

d Ayu 12:19

e 1Sa 2:7

f 1Sa 2:5
Zb 34:10
Zb 107:9

g Zb 98:3
Isa 41:8,9

h Mwa 17:19
Mik 7:20
Gal 3:16

i Lu 1:14

j Mwa 17:10,12
Law 12:2,3

k Lu 1:13

l Lu 1:20

mambo makuu, nalo jina lake ni takatifu,^a **50** naye huwao-nyesha rehema wale wanao-mwogopa, kizazi baada ya kizazi.^b **51** Amefanya mambo makuu kwa mkono wake, amewatawanya wenye majivuno katika nia ya mioyo yao.^c **52** Amewashusha watu wenye nguvu kutoka kwenye viti vya ufalme^d na kuwainua watu wa hali ya chini;^e **53** amewashibisha kabisa wenye njaa kwa vitu vyema^f na kuwafukuza mikono mitupu wale waliokuwa na mali. **54** Amekuja kumsaidia Israeli mtumishi wake, amekumbuka rehema zake,^g **55** kama alivyowaahidi mababu zetu, Abrahamu na uzao wake,^{*h} milele.” **56** Maria akakaa na Elisabeti kwa karibu miezi mitatu, kisha akarudi nyumbani kwake.

57 Wakati wa Elisabeti wa kujifungua ukafika, naye akazaa mtoto wa kiume. **58** Majirani na watu wake wa ukoo wakasikia kwamba Yehova* amemwonyesha rehema nyi-nyi, wakafurahi pamoja naye.ⁱ **59** Siku ya nane wakaja kumtahiri huyo mtoto,^j nao wali-taka kumpa jina la baba yake, Zekaria. **60** Lakini mama yake akajibu: “Hapana! ataitwa Yohana.” **61** Wakamwambia: “Hakuna mtu wenu wa ukoo anayeitwa jina hilo.” **62** Kisha wakamuuliza baba yake wakitumia ishara jina alilotaka kumpa. **63** Basi akomba kibao akaandika: “Yohana ndilo jina lake.”^k Ndipo wote wakashangaa. **64** Mara moja kinywa chake kikafunguliwa na ulimi wake ukawe-kwa huru, akaanza kuongea,^l

1:55 *Tnn., “mbegu yake.”

akimsifu Mungu. **65** Majirani wao wote wakaogopa, na mambo yote hayo yakaa-nza kuzungumziwa katika eneo lote la milimani la Yudea. **66** Wote waliosikia mambo hayo wakayaweka moyoni, wakisema: "Mtoto huyu atakuwa mtu wa aina gani?" Kwa maana mkono wa Yehova* ulikuwa pamoja naye.

67 Kisha Zekaria baba yake akajazwa roho takatifu, naye akatoa unabii huu: **68** "Asifiwe Yehova* Mungu wa Israeli,^a kwa sababu amewakumbuka watu wake na kuwaletea ukombozi.^b **69** Naye ametu-nulia pembe ya wokovu*^c katika nyumba ya Daudi mtu-mishi wake,^d **70** kama alivyosema kupitia kinywa cha manabii wake watakatifu tangu zamani.^e **71** kwa-mba atatuokoa kutoka kwa adui zetu na kutoka mikononi mwa wote wanaotuchukia;^f **72** ili kuonyesha rehema kuhusiana na mababu zetu na kulikumbuka agano lake takatifu,^g **73** kama alivyomw-pia Abrahamu babu yetu,^h **74** kwamba atatukombo- kutoka mikononi mwa adui, na kutupatia pendeleo la kumto- lea utumishi mtakatifu bila woga **75** kwa ushikamanifu na uadilifu mbele zake siku zetu zote. **76** Lakini wewe, mtoto mchanga, utaitwa nabii wa Aliye Juu Zaidi, kwa maana utaenda mbele za Yehova* ili kutayarisha njia zake,ⁱ **77** kuwapa watu wake ujuzi wa wokovu kupitia kusamehe- wa dhambi zao,^j **78** kwa sa-

1:66, 68, 76; 2:9 * Angalia Nyongeza A5. 1:69 * Au "mwokozi mwenye nguvu." Angalia Kamusi, uku. 2012, "Pembe."

SURA YA 1

a 1Fa 1:48
Zb 41:13
Zb 72:18
Zb 106:48

b Zb 111:9
Lu 7:16

c 1Sa 2:10

d Zb 132:17

e Yer 23:5
Da 9:24

f Zb 106:10

g Mwa 17:7
Law 26:42
Zb 106:45, 46

h Mwa 22:15-18
Zb 105:8, 9
Mik 7:20

i Isa 40:3
Mal 3:1
Mt 3:3

j Mk 1:4

Safu ya 2

a Zb 107:10
Isa 9:2
Mt 4:16

SURA YA 2

b Mt 1:16

c 1Sa 16:1
Mik 5:2
Mt 2:6

d Lu 1:26, 27

e Mt 1:18

f Mt 1:25

g Isa 53:2

babu ya huruma nyororo za Mungu wetu. Kwa huruma hizo tutapata mapambazu-ko kutoka juu, **79** ili kuwapa nuru wale wanaokaa gizani na katika kivuli cha kifo^a na kuo- ngoza hatua zetu kwenye njia ya amani."

80 Yule mtoto akakua na kupata nguvu katika roho, naye aliishi jangwani mpaka siku aliyojionyesha waziwazi kwa Israeli.

2 Basi katika siku hizo Kai- sari Augusto alitoa amri kwamba watu wote wa dunia inayokaliwa waandikishwe. **2** (Uandikishaji huo wa kwanza ulifanyika Kirenio alipo- kuwa gavana wa Siria.) **3** Na watu wote wakaenda kuandi- kishwa kila mmoja katika jiji lake. **4** Yosefu^b pia akatoka jiji la Nazareti huko Galila- ya akapanda kwenda Yudea katika jiji la Daudi, linaloi- twa Bethlehemu,^c kwa sababu alikuwa wa nyumba na familia ya Daudi. **5** Alienda kuandi- kishwa pamoja na Maria amba- ye alikuwa amemwoa kama ili- vyoahidiwa,^d naye alikuwa ka- ribu kuzaa.^e **6** Wakiwa huko, wakati wake wa kuzaa ukafika. **7** Naye akamzaa mwana, mza- liwa wake wa kwanza,^f aka- mfunga kwa vitambaa na ku- mlaza katika hori,^g kwa saba- bu hawakupata nafasi katika nyumba za wageni.

8 Kulikuwa pia na wachu- ngaji katika eneo hilo ambao waliishi nje wakichunga ma- kundi yao usiku. **9** Ghafila malaika wa Yehova* akawa- tokea, na utukufu wa Yehova* ukawaangazia pande zote, nao wakaogopa sana. **10** La- kini malaika akawaambia:

“Msiogope, kwa maana tazama! ninawatangazia habari njema ya shangwe kubwa ambayo watu wote watakuwa nayo. **11** Kwa sababu leo katika jiji la Daudi,^a amezaliwa mwokozi^b ambaye ni Kristo, Bwana.^c **12** Na hii ndiyo ishara kwenu: Mtamkuta mto to aliyefungwa kwa vitambaa akiwa amelala katika hori.” **13** Ghafla wakaona umati wa jeshi la mbinguni ukiwa pamoja na yule malaika,^d wakimsifu Mungu wakisema: **14** “Utukufu kwa Mungu katika vilele vilivyo juu, na amani duniani kwa watu wenye nia njema.”* **15** Baada ya malaika kurudi mbinguni, wachungaji wakaanza kuambiana: “Twendeni Bethlehemu tukaone jambo hili ambalo Yehova* ametujulisha.” **16** Wakaenda haraka wakamkuta Maria na Yosefu, na yule mtoto mchanga akiwa amelala katika hori. **17** Walipoona jambo hilo, wakawaeleza ujumbe walioambiwa kuhusu mtoto huyo mchanga. **18** Wote waliosikia wakashangazwa na mambo waliyoambiwa na wachungaji, **19** lakini Maria akaanza kuyahifadhi maneno hayo yote, na kukata kauli moyoni mwake.^e **20** Basi wachungaji wakarudi, wakimtukuza na kumsifu Mungu kwa sababu ya mambo yote walivyosikia na kuona, kama tu walivyokuwa wameambiwa.

21 Baada ya siku nane, wakati ulipofika wa kumtahiri,^f wakampa jina Yesu, jina alilopewa na malaika kabla ya Maria kupata mimba.^g

2:14 *Au “watu wenye kibali chake.”
2:15, 22-24, 26 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 2

a 1Sa 20:6

b Isa 9:6

c Mdo 2:36
Flp 2:11d Da 7:10
Ufu 5:11

e Lu 2:51

f Mwa 17:10, 12
Law 12:2, 3g Mt 1:20, 21
Lu 1:30, 31

Safu ya 2

a Law 12:2, 4

b Kut 13:2, 12
Kut 22:29
Hes 3:13
Hes 8:17

c Law 12:6, 8

d Isa 40:1
Isa 49:13

e Law 12:6, 7

f Mwa 46:30

g Isa 52:10
Lu 3:4, 6
Mdo 4:12

h Isa 40:5

i Isa 9:2
Mt 4:16j Isa 11:10
Isa 42:6
Isa 49:6
Mdo 13:47
Mdo 26:23

22 Pia, wakati ulipofika wa kuwatakaswa kulingana na Sheria ya Musa,^a wakamleta Yerusalemu ili kumtoa kwa Yehova,^{*} **23** kama ilivyoandikwa katika Sheria ya Yehova: “Kila mzaliwa wa kwanza^h wa kiume lazima ataitwa mtakatifu kwa Yehova.”*^b

24 Wakatoa dhabihu kama ilivyoandikwa katika Sheria ya Yehova: “njiwa tetere wawili au hua wawili wachanga.”^c

25 Na tazama! kulikuwa na mtu fulani Yerusalemu aliyetwa Simeoni, alikuwa mwadilifu na alimwogopa Mungu, naye alikuwa akisubiri faraja ya Israeli,^d na roho takatifu ilikuwa juu yake. **26** Zaidi ya hayo, Mungu alikuwa amemfunulia kupitia roho takatifu kwamba hangekufa kabla ya kumwona Kristo wa Yehova.* **27** Akaja hekaluni akiongozwa na roho, na wazazi wa yule mtoto Yesu walipomleta ili kufanya kulingana na desturi ya Sheria,^e **28** akambeba yule mtoto mikononi mwake akamsifu Mungu akisema: **29** “Sasa, Bwana Mwenye Enzi Kuu, unaruhusu mtumwa wako aende kwa amani^f kulingana na tangazo lako, **30** kwa sababu macho yangu yameona njia yako ya kuleta wokovu^g **31** ambayo umetayarisha machoni pa watu wote,^h **32** nuruⁱ ya kuondoa kitambaa* kwa mataifa^j na utukufu wa watu wako Israeli.” **33** Baba na mama ya yule mtoto wakaendelea kushangazwa na mambo yaliyokuwa yakisemwa kumhusu. **34** Pia, Simeoni akawabariki

2:23 *Tnn., “anayefungua tumbo la uza-zi.” 2:32 *Au “utaji.”

na kumwambia Maria, mama ya yule mtoto: “Tazama! Mto-to huyu amewekwa rasmi kwa ajili ya kuanguka^a na kuinuka tena kwa wengi katika Israe-^bli^b na kuwa ishara itakayose-^cliwa vibaya^c 35 (ndiyo, upa-^dnga mrefu utakuchoma*),^d ili mawazo ya mioyo mingi yafu-^enuliwe.”

36 Kulikuwa na nabii wa kike aliyelitwa Ana, binti ya Fanueli, wa kabila la Ashe-^fri, ambaye alikuwa amezeeka. Alikuwa ameishi na mume wake kwa miaka saba baada ya kuolewa,* 37 na sasa alikuwa mjane mwenye umri wa miaka 84. Hakukosa kamwe hekaluni, akitoa utumishi mta-^gkatifu usiku na mchana, aki-^hfunga na kutoa dua. 38 Wa-ⁱkati huohuo, akaja na kuanza kumshukuru Mungu akiwaa-^jmbia kuhusu mtoto huyo wale wote waliokuwa wakisubiri ukombozi wa Yerusalemu.^e

39 Basi, baada ya kufanya mambo yote kulingana na Sheria ya Yehova,*^f wakaru-^gdi huko Galilaya kwenye jiji la kwao la Nazareti.^g 40 Yule mtoto akaendelea kukua na kupata nguvu, akazidi kuwa na hekima, na akaendelea kuwa na kibali cha Mungu.^h

41 Wazazi wake walikuwa na desturi ya kwenda Yeru-ⁱsalemu kila mwaka kwa ajili ya sherehe ya Pasaka.ⁱ 42 Na alipokuwa na umri wa miaka 12, wakapanda kwenda kuli-^jngana na desturi ya shere-^khe.^j 43 Siku za sherehe zilipokwisha wakaanza kuru-^ldi nyumbani, lakini mvula-

2:35 *Au “utakuchoma nafsi yako.”
2:36 *Tnn., “tangu alipokuwa bikira.”
2:39 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 2

a Isa 8:14

b 1Ko 1:23, 24

c Mdo 28:22
1Pe 2:7, 8

d Yoh 19:25

e Isa 52:9
Mk 15:43
Lu 2:25

f Law 12:6

g Mt 2:23
Lu 1:26

h Lu 2:52

i Kut 23:14, 15
Kum 16:16

j Kut 34:23

Safu ya 2

a Zb 119:99
Mt 7:28
Mk 1:22
Yoh 7:15

b Yoh 2:16

c Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:1
Kol 3:20

d Lu 2:19

SURA YA 3

e Mt 14:1
Lu 23:6, 7

na Yesu akabaki Yerusalemu, hata hivyo, wazazi wake hawa-^akujua. 44 Walisafiri umbali wa siku moja wakidhani Yesu alikuwa miongoni mwa wasa-^bfiri, kisha wakaanza kumta-^cfuta kati ya watu wao wa ukoo na watu waliowafaha-^dmu. 45 Walipomkosa waka-^erudi mpaka Yerusalemu na ku-^fmtafuta kwa bidii. 46 Baada ya siku tatu wakampata he-^gkaluni akiwa ameketi katika-^hti ya walimu akiwasikiliza na kuwauliza maswali. 47 Laki-ⁱni wote waliomsikiliza waliku-^jwa wakishangazwa na majibu yake na uwezo wake wa kuele-^kwa.^a 48 Wazazi wake walipo-^lmwona wakashangaa, mama yake akamwambia: “Mwana-^mngu, kwa nini umetutendea hivi? Mimi na baba yako tu-ⁿmekuwa tukikutafuta tukiwa na wasiwasi mwingi.” 49 La-^okini akawaambia: “Kwa nini mlikuwa mkinitafuta? Je, ha-^pmkujua kwamba ninapaswa kuwa katika nyumba ya Baba yangu?”^b 50 Hata hivyo, ha-^qwakuelewa mambo aliyoku-^rwa akiwaambia.

51 Yesu akashuka pamo-^sja nao kurudi Nazareti, akae-^tndelea kuwatii.*^c Naye mama yake akayahifadhi kwa unga-^ulifu mambo hayo yote moyoni mwake.^d 52 Yesu akaende-^vlea kukua na kupata hekima zaidi, pia akazidi kupata kiba-^wli cha Mungu na wanadamu.

3 Katika mwaka wa 15 wa utawala wa Kaisari Tibe-^xrio, Pontio Pilato alipokuwa gavana wa Yudea, Herode*^e alipokuwa mtawala wa wila-

2:51 *Au “akabaki mtiifu.” 3:1 *Yaa-
ni, Herode Antipa. Angalia Kamusi,
uku. 2012.

ya* ya Galilaya, Filipino ndugu yake alipokuwa mtawala wa wilaya ya Iturea na Trakoni, naye Lisania alipokuwa mtawala wa wilaya ya Abilene, 2 katika siku za Kayafa^a na mkuu wa makuhani Anasi, Yohana^b mwana wa Zekaria akiwa nyikani, alipokea ujumbe kutoka kwa Mungu.^c

3 Basi akaenda katika maeneo yote yaliyokuwa kariibu na Yordani, akiwahubiria watu wabatizwe ili kuonyesha kwamba wametubu na hivyo wasamehewe dhambi zao,^d 4 kama ilivyoandikwa katika kitabu cha maneno ya nabii Isaya: “Kuna mtu anayepaza sauti nyikani: ‘Tayarishe ni njia ya Yehova!’ Nyooshe ni barabara zake.”^e 5 Lazima kila bonde lijazwe, na kila mlima na kilima visawazishwe; lazima barabara zilizopinda zinyooshwe, na barabara zenye miparuzo zilainishwe; 6 na wote wenye mwili* wataona wokovu wa Mungu.”^f

7 Basi akaanza kuuambia umati uliokuja kwake ili awabatize: “Enyi uzao wa nyoka,* ni nani amewaonya mki-mbie ghadhabu inayokuja?^g 8 Basi zaeni matunda nayoonyesha toba. Wala msijiambie, ‘Abrahamu ndiye baba yetu.’ Kwa maana ninawaambia, Mungu anaweza kumwinulia Abrahamu watoto kutoka kwenye mawe haya. 9 Kwa kweli, tayari shoka limewekwa kwenye mzizi wa miti. Basi, kila mti usiozaa matunda mazuri utakatwa na kutupwa motoni.”^h

3:1 *Tnn., “tetraki.” 3:4 *Angalia Nyoongeza A5. 3:6 *Au “wanadamu wote.”^a Au “njia ya Mungu ya kuokoa.” 3:7 *Au “nyoka-vipiri.”

SURA YA 3

a Mt 26:57
Yoh 18:13
Yoh 18:24
Mdo 4:5, 6

b Yoh 1:6

c Lu 1:80

d Mt 3:1, 2
Mk 1:4
Lu 1:76, 77

e Mt 3:3
Mk 1:3
Yoh 1:23

f Isa 40:3-5
Lu 2:30
Mdo 28:28

g Mt 3:7-10
Mt 23:33

h Mt 7:19

Safu ya 2

a 1Ti 6:18
Yak 2:15, 16
1Yo 3:17

b Mt 21:32
Lu 7:29

c Lu 19:8

d Kut 23:1, 7
Law 19:11

e Yoh 1:25

f Yoh 1:26, 27

g Mt 3:11, 12
Mk 1:7, 8
Mdo 2:1, 4

10 Umati ulikuwa ukimuuliza: “Basi, tufanye nini?”

11 Akawajibu: “Mtu aliye na mavazi mawili* ampe vazi moja yule ambaye hana, na aliye na chakula afanye vi-vyo hivyo.”^a 12 Hata wakusanya kodi wakaja ili wabatizwe,^b wakamuuliza: “Mwalimu, tufanye nini?” 13 Akawaambia: “Msidai* zaidi ya kiwango kilichowekwa cha kodi.”^c 14 Pia, wale walio katika utumishi wa jeshi walikuwa wakimuuliza: “Tufanye nini?” Akawaambia: “Msimsumbue* mtu yeyote wala kumshtaki mtu yeyote kwa uwongo,^d bali mtosheke na posho yenu.”[#]

15 Kwa kuwa watu walikuwa wakitarajia, wote walikuwa wakijiuliza moyoni mwao kuhusu Yohana, “Je, labda huyu ndiye Kristo?”^e 16 Yohana akawajibu: “Mimi ninawabatiza kwa maji, lakini anakuja mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye sistahili ku-fungua kamba za viatu vyake.^f Yeye atawabatiza kwa roho takatifu na moto.^g 17 Sepetu yake ya kupepetea imo mkononi mwake ili kuusafisha kabisa uwanja wake wa kupuria, na kukusanya ngano katika ghala lake, lakini atayateketeza makapi kwa moto usioweza kuzimwa.”

18 Pia, aliwahimiza kwa maneno mengine mengi na akaendelea kuwatangazia watu habari njema. 19 Yohana alikuwa amemkaripia Herode mtawala wa wilaya kwa kumchukua Herodia mke wa ndugu yake na kwa sababu ya

3:11 *Au “vazi la ziada.” 3:13 *Au “Msi-kusanye.” 3:14 *Au “Msimdhulumu.”[#] Au “mishahara yenu.”

matendo yote maovu ambayo Herode alikuwa amefanya, **20** aliongeza hili pia kwenye matendo hayo yote: Alimfunga Yohana gerezani.^a

21 Baada ya watu wote kubatizwa, Yesu pia akabatizwa.^b Alipokuwa akisali, mbingu zikafunguka,^c **22** roho takatifu ikashuka juu yake ikiwa na umbo kama la njiwa, na sauti ikasikika kutoka mbinguni ikisema: "Wewe ni Mwanangu, mpendwa; nimekukubali."^d

23 Yesu^e alikuwa na umri wa miaka 30 hivi alipoanza kazi yake,^f akiwa mwana, kama alivyoona,

wa Yosefu,^g

mwana wa Heli,

24 mwana wa Mathati,

mwana wa Lawi,

mwana wa Melki,

mwana wa Yanai,

mwana wa Yosefu,

25 mwana wa Matathia,

mwana wa Amosi,

mwana wa Nahumu,

mwana wa Esli,

mwana wa Nagai,

26 mwana wa Maathi,

mwana wa Matathia,

mwana wa Semei,

mwana wa Yoseki,

mwana wa Yoda,

27 mwana wa Yonani,

mwana wa Rea,

mwana wa Zerubabeli,^h

mwana wa Shealtiel,ⁱ

mwana wa Neri,

28 mwana wa Melki,

mwana wa Adi,

mwana wa Kosamu,

mwana wa Elmadamu,

mwana wa Eri,

29 mwana wa Yesu,

mwana wa Eliezeri,

mwana wa Yorimu,

SURA YA 3

a Mt 14:3-5

Mk 6:17-20

b Mt 3:13

c Mt 3:16

Mk 1:9, 10

d Zb 2:7

Mt 3:17

Mt 17:5

Mk 1:11

Yoh 1:32-34

e Mt 1:1-17

f Hes 4:2, 3

g Mt 1:16

Mt 13:55

Lu 4:22

Yoh 6:42

h Ezr 3:2

i 1Nya 3:17

Mt 1:12

Safu ya 2

a 2Sa 5:13, 14

1Nya 3:5

b 1Sa 16:13

1Sa 17:58

Mt 1:6

c Isa 11:1

d Ru 4:17

e Ru 4:13

f Ru 4:21

g 1Nya 2:11

h Ru 4:12

Ru 4:18, 19

1Nya 2:4, 5

i Mwa 29:35

1Nya 2:1

j Mwa 25:26

k Mwa 21:2, 3

l 1Nya 1:28

m Mwa 11:24

Mwa 11:26, 27

n Mwa 11:22

o Mwa 11:20

p Mwa 11:18

q Mwa 11:16

r Mwa 11:14

1Nya 1:25

s Mwa 11:12

t Mwa 11:10

u Mwa 5:32

v Mwa 5:29

w Mwa 5:25

x Mwa 5:21

y Mwa 5:19

z Mwa 5:12, 16

a Mwa 5:9

1Nya 1:2

b Mwa 4:26

Mwa 5:10

c Mwa 5:7

d Mwa 5:1, 4

1Nya 1:1

mwana wa Mathati,

mwana wa Lawi,

30 mwana wa Simioni,

mwana wa Yuda,

mwana wa Yosefu,

mwana wa Yonamu,

mwana wa Eliakimu,

31 mwana wa Melea,

mwana wa Mena,

mwana wa Matatha,

mwana wa Nathani,^a

mwana wa Daudi,^b

32 mwana wa Yese,^c

mwana wa Obedi,^d

mwana wa Boazi,^e

mwana wa Salmoni,^f

mwana wa Nashoni,^g

33 mwana wa Aminadabu,

mwana wa Arni,

mwana wa Hezroni,

mwana wa Perezi,^h

mwana wa Yuda,ⁱ

34 mwana wa Yakobo,^j

mwana wa Isaka,^k

mwana wa Abrahamu,^l

mwana wa Tera,^m

mwana wa Nahori,ⁿ

35 mwana wa Serugi,^o

mwana wa Reu,^p

mwana wa Pelegi,^q

mwana wa Eberi,^r

mwana wa Shela,^s

36 mwana wa Kainani,

mwana wa Arpakhshadi,^t

mwana wa Shemu,^u

mwana wa Noa,^v

mwana wa Lameki,^w

37 mwana wa Methusela,^x

mwana wa Enoko,

mwana wa Yaredi,^y

mwana wa Mahalaleeli,^z

mwana wa Kainani,^a

38 mwana wa Enoshi,^b

mwana wa Sethi,^c

mwana wa Adamu,^d

mwana wa Mungu.

4 Basi Yesu, akiwa ame-
jaa roho takatifu, akaon-
doka Yordani, naye akaongo-
zwa na roho kwenda nyikani^a
2 kwa siku 40, akijaribiwa
na Ibilisi.^b Kipindi hicho cho-
te hakula chakula, basi muda
huo ulipokwisha, akahisi njaa.
3 Ndipo Ibilisi akamwambia:
“Ikiwa wewe ni mwana wa Mu-
ngu, liambie jiwe hili liwe mka-
te.” **4** Lakini Yesu akamjibu:
“Imeandikwa, ‘Mwanadamu
hataishi kwa mkate tu.’”^c

5 Basi akampeleka juu na
kumwonyesha mara moja fal-
me zote za dunia inayokaliwa.^d

6 Kisha Ibilisi akamwambia:
“Nitakupa mamlika yote hii
na utukufu wake, kwa sababu
nimepewa,^e nami humpa ye-
yote ninayetaka. **7** Kwa hiyo,
ukifanya tendo la ibada mbe-
le yangu, yote itakuwa yako.”
8 Yesu akamjibu: “Imeandi-
kwa, ‘Yehova* Mungu wako
ndiye unayepaswa kumwabu-
du na yeye peke yake ndiye
unayepaswa kumtolea utumi-
shi mtakatifu.’”^f

9 Kisha akampeleka Yerusa-
lemu, akamsimamisha juu ya
mnara wa* hekalu na kumwa-
mbia: “Ikiwa wewe ni mwana
wa Mungu, jitupe chini ku-
toka hapa,^g **10** kwa maana
imeandikwa, ‘Atawaagiza ma-
laika zake kukuhusu wewe,
ili wakulinde,’ **11** nao, ‘Wa-
takubeba mikononi mwao, ili
mguu wako usigonge jiwe.’”^h
12 Yesu akamjibu: “Imese-
mwa, ‘Usimjaribu Yehova* Mu-
ngu wako.’”ⁱ **13** Kwa hiyo Ibi-
lisi, alipomaliza majaribu yote,

4:8, 12, 18, 19 *Angalia Nyongeza A5.
4:9 *Au “ukuta wa ukingoni wa; sehemu
ya juu zaidi ya.”

SURA YA 4

a Mt 4:1-4
Mk 1:12, 13

b Ebr 2:18

c Kum 8:3

d Mt 4:8-10

e Yoh 12:31
Yoh 14:30
Efe 2:2

f Kut 20:3
Kum 6:13
Kum 10:20

g Mt 4:5-7

h Zb 91:11, 12

i Kum 6:16
1Ko 10:9

Safu ya 2

a Mt 4:11
Ebr 4:15

b Mt 4:12
Yoh 4:3

c Mt 2:23

d Mdo 17:1, 2

e Mt 12:20

f Isa 61:1, 2

g Mt 5:17

h Zb 45:2
Isa 50:4

i Mt 13:54
Mk 6:2
Yoh 6:42

akamwacha mpaka wakati
mwingine unaofaa.^a

14 Basi Yesu akarudi Gali-
laya^b katika nguvu za roho. Na
habari nzuri kumhusu zika-
nea katika maeneo yote yali-
yo karibu. **15** Pia, akaanza
kufundisha katika masinago-
gi yao, naye akaheshimiwa na
watu wote.

16 Kisha akaenda Nazareti,^c
mahali alipolelewa, na kuli-
ngana na desturi yake siku ya
Sabato, akaingia katika sina-
gogi^d naye akasimama ili kusoma.
17 Basi akapewa kitabu
cha kukunjwa cha nabii Isaya,
akakifungua na kupata mahali
palipoandikwa: **18** “Roho ya
Yehova* iko juu yangu, kwa sa-
babu alinitia mafuta ili niwa-
tangazie maskini habari nje-
ma. Alinituma niwatangazie
mateka uhuru na vipofu kuo-
na tena, kuwaweka huru wali-
liopondeka,^e **19** kuhubiri
mwaka wa Yehova* unaoku-
balika.”^f **20** Ndipo akakiku-
nja kitabu hicho na kumrudi-
shia mtumishi, kisha akaketi;
na wote katika sinagogi wali-
kuwa wakimtazama kwa maki-
ni. **21** Akaanza kuwaambia:
“Leo andiko hili ambalo mme-
toka kusikia limetimia.”^g

22 Wote wakaanza kutoa
ushahidi unaofaa kumhu-
su na kushangazwa na ma-
neno yenye neema yaliyoku-
wa yakitoka kinywani mwa-
ke,^h nao wakawa wakiambi-
ana: “Huyu ni mwana wa
Yosefu, sivyo?”ⁱ **23** Ndipo
akawaambia: “Bila shaka
mtautumia mfano huu kwa-
ngu, ‘Daktari, jiponye mwe-
nyewe. Fanya pia katika eneo
la nyumbani kwenu mambo
tuliyosikia yamefanywa huko

Kapernaumu.”^a **24** Basi aka-waambia: “Kwa kweli nina-waambia hakuna nabii anaye-kubaliwa katika eneo la nyu-mbani kwao.^b **25** Kwa mfa-no, kwa kweli ninawaambia: Kulikuwa na wajane wengi Israeli siku za Eliya, mbingu zilipofungwa kwa miaka mita-tu na miezi sita, kukawa na njaa kubwa katika nchi yote.^c **26** Lakini Eliya hakutumwa kwa yeyote kati ya wanawa-ke hao, bali kwa mjane mmo-ja huko Sarefathi katika nchi ya Sidoni.^d **27** Pia, kulikuwa na wenye ukoma wengi Israe-li siku za nabii Elisha; lakini hakuna hata mmoja wao ali-yetakaswa,* ila Naamani Msi-ria.”^e **28** Ndipo wote katika sinagogi waliokuwa wakisikia mambo hayo wakajawa na ha-sira,^f **29** wakasimama na ku-mtoa haraka nje ya jiji mpa-ka kwenye ukingo wa mlima ambao jiji lao lilikuwa limeje-ngwa, ili wamtupe chini. **30** Lakini akapita katikati yao na kwenda zake.^g **31** Kisha akashuka kwenda jiji la Kapernaumu, huko Gal-ilaya. Naye alikuwa akiwa-fundisha siku ya Sabato,^h **32** nao wakashangazwa na njia yake ya kufundisha,ⁱ kwa sababu alikuwa akizungu-mza kwa mamlaka. **33** Basi katika sinagogi kulikuwa na mtu mwenye roho mwo-vu, naye akapiga kelele aki-sema: **34** “Ah! Kwa nini unat-uzumbua, wewe Yesu Mna-zareti?^k Je, umekuja ku-tuangamiza? Ninajua wewe ni nani, Mtakatifu wa Mungu.”^l **35** Lakini Yesu akamkemea, akisema: “Nyamaza na umto-

4:27 *Au “aliyeponywa.”

SURA YA 4

- a Mt 4:13
- b Mt 13:57
Mk 6:4
Yoh 4:44
- c 1Fa 18:1
- d 1Fa 17:9,10
- e 2Fa 5:1,14
- f Lu 2:34
- g Yoh 8:59
Yoh 10:39
- h Mk 1:21,22
- i Mt 7:28
Yoh 7:46
- j Mk 1:23-28
- k Mt 2:23
- l Mt 8:29
Lu 4:41
Lu 8:28
Yak 2:19

Safu ya 2

- a Mt 8:14,15
Mk 1:29-31
- b Mt 8:16,17
Mk 1:32-34
- c Mt 8:28,29
Mk 3:11
- d Mdo 16:17,18
- e Mk 1:23-25
Mk 3:11,12
Lu 4:33-35
- f Mt 1:35-38
- g Mt 4:23
Lu 8:1

ke.” Basi baada ya kumwangu-sha mtu huyo mbele yao, yule roho mwovu akamtoka bila kumuumiza. **36** Wote waka-shangaa na kuanza kuambia-na: “Anazungumza kwa mam-laka sana! Anawaagiza roho waovu kwa mamlaka na ngu-vu, nao wanatoka!” **37** Basi habari kumhusu zikazidi kue-nea kila mahali katika maeneo yaliyokuwa karibu.

38 Alipotoka katika sinago-gi akaenda nyumbani kwa Sim-oni. Mama mkwe wa Simo-ni alikuwa na homa kali, wa-kamwomba Yesu amponye.^a **39** Yesu akasimama kando yake, akaikemea ile homa, ikaisha. Papo hapo akasima-ma na kuanza kuwahudumia.

40 Jua lilipokuwa likitua, wote waliokuwa na watu we-nye magonjwa mbalimbali wa-kawaleta kwake. Akawaponya kwa kuweka mikono yake juu ya kila mgonjwa.^b **41** Roho waovu pia wakawatoka watu wengi, wakipaza sauti na ku-sema: “Wewe ndiye Mwana wa Mungu.”^c Lakini aliwakemea na hakuwaruhusu waseme,^d kwa maana walijua yeye ni Kristo.^e

42 Hata hivyo, kulipopa-mbazuka, akaenda mahali pa-sipo na watu.^f Lakini umati ukaanza kumtafuta* na wali-pofika mahali alipokuwa, wa-kajaribu kumzuia asiondoke. **43** Lakini akawaambia: “Ni lazima pia nitangaze haba-ri njema ya Ufalme wa Mungu katika majiji mengine, kwa sa-babu nilitumwa kufanya hi-vyo.”^g **44** Basi akaendelea kuhubiri katika masinagogi ya Yudea.

4:42 *Au “kumwinda”

5 Pindi moja, Yesu alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti*^a na umati ulikuwa umemsonga ili kusikiliza neno la Mungu. **2** Akao-na mashua mbili zikiwa zimeegeshwa kando ya ziwa, lakini wavuvi walikuwa wametoka na walikuwa wakiosha nyavu zao.^b **3** Akaingia katika mashua moja iliyokuwa ya Simoni, akamwomba aivute mballi kidogo na nchi kavu. Kisha akaketi na kuanza kuwafundisha watu akiwa kwenye mashua. **4** Alipoacha kuzungumza, akamwambia Simoni: “Peleka mashua mahali penye kina, kisha mshushe nyavu zenu, mvue samaki.” **5** Simoni akamjibu: “Mwalimu, tumejitahidi kuvua samaki usiku wote na hatukupata chochote,^c lakini nitazishusha nyavu kama ulivyoniagiza.” **6** Basi walipofanya hivyo, wakavua* samaki wengi sana hivi kwamba nyavu zao zikaanza kukatika.^d **7** Wakawaita wenzao waliokuwa katika ile mashua nyingine waje kuwasaidia, waka-na kuajaza mashua zote mbili, nazo zikaanza kuzama. **8** Simoni Petro alipoona hivyo, akaanguka magotini pa Yesu na kusema: “Bwana ondoka kwangu, kwa sababu mimi ni mtu mwenye dhambi.” **9** Kwa maana yeye na wenzake walishangazwa sana na samaki wengi waliovua. **10** Pia, Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo,^e ambao walishirikiana na Simoni wakashangaa. Lakini Yesu akamwambia Simoni: “Acha kuogopa. Kuanzia sasa utakuwa ukiwavua watu

5:1 *Yaani, Bahari ya Galilaya. 5:6 *Tnn., “wakazingira.”

SURA YA 5

a Mt 4:18
Mk 1:16

b Mt 4:21

c Yoh 21:3

d Yoh 21:6

e Mt 4:21
Mk 1:19

Safu ya 2

a Mt 4:19
Mk 1:17

b Mt 4:20
Mt 6:33
Mt 19:27
Mk 1:20
Lu 18:28
Flp 3:8

c Mt 8:2
Mk 1:40-45

d Mt 8:3
Mk 1:41

e Law 14:2-4
Law 14:10, 20

f Mt 8:4

g Mt 4:24, 25
Mk 3:7, 8
Yoh 6:2

h Mk 2:1, 2

i Mt 9:2
Mk 2:3-12

wakiwa hai.”^a **11** Basi wakarudisha mashua kwenye nchi kavu, wakaacha kila kitu na kumfuata.^b

12 Pindi nyingine alipokuwa katika jiji fulani, tazama! kulikuwa na mwanamume aliyejaa ukoma! Alipomwona Yesu, akajianguka kifudufudi na kumwomba: “Bwana, ikiwa tu unataka, unaweza kunitakasa.”^c **13** Basi Yesu akanyoosha mkono wake akamgusa na kusema: “Ninataka! Takasika.” Mara moja ule ukoma ukaisha.^d **14** Kisha akamwagiza mtu huyo asimwambie mtu yeyote: “Bali nenda ukajionyeshe kwa kuhani, kisha utoe toleo la kutakaswa kwako, kama alivyoagiza Musa,^e ili kuwa ushahidi kwao.”^f **15** Lakini habari kumhusu zikazidi kuenea, na umati mkubwa ulikuwa ukikusanyika ili kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao.^g **16** Hata hivyo, mara kwa mara alienda mahali pasipo na watu ili kusali.

17 Siku moja alipokuwa akifundisha, Mafarisayo na walimu wa sheria kutoka kila kiji-ji cha Galilaya na Yudea na kutoka Yerusalemu walikuwa wameketi hapo; na Yehova* alikuwa amempa nguvu za kuponya.^h **18** Na tazama! kulikuwa na wanaume waliombeba kwenye kitanda* mtu aliyepooza, nao wakaribu kumwingiza ndani na kumweka mbele ya Yesu.ⁱ **19** Waliposhindwa kumwingiza kwa sababu ya umati, wakapanda kwenye paa, wakaondoa vigae na kumshusha

5:17 *Angalia Nyongeza A5. 5:18 *Au “machelu.”

akiwa kwenye kitanda kati ya wale waliokuwa mbele ya Yesu.

20 Alipoona imani yao, akamwambia yule mtu: “Ewe mtu, umesamehewa dhambi zako.”^a

21 Ndipo waandishi na Mafarisayo wakaanza kujadiliana: “Huyu ni nani anayesema makufuru? Ni nani anayeweza kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake?”^b

22 Lakini Yesu, akifahamu mawazo yao akawauliza: “Mnawaza nini katika mioyo yenu?”

23 Ni jambo gani rahisi zaidi kusema, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema, ‘Simama utembe?’

24 Lakini ili mjue kwamba Mwana wa binadamu ana mamlaka ya kusamehe dhambi duniani—” akamwambia yule mtu aliyepoza: “Ninakuambia, Simama, uchukue kitanda chako, uende nyumbani.”^c

25 Ndipo akasimama mbele yao, akachukua kitanda chake, akaenda nyumbani, akimtukuza Mungu. **26** Kisha wote wakashangaa wakaanza kumtukuza Mungu, wakastaajabu na kusema: “Leo tumeona mambo ya ajabu!”

27 Baada ya mambo hayo akaenda nje na kumwona mkusanya kodi anayelitwa Lawi akiwa ameketi kwenye ofisi ya kodi, akamwambia: “Njoo uwe mfuasi wangu.”^d

28 Naye akasimama, akaacha kila kitu na kuanza kumfuata.

29 Kisha Lawi akamwandalia Yesu karamu kubwa nyumbani kwake, na kulikuwa na umati mkubwa wa waku-sanya kodi na wengine waliokuwa wakila* pamoja nao.^e

30 Ndipo Mafarisayo na waa-

SURA YA 5

a Mt 9:2-8

b Zb 103:2,3
Zb 130:3,4
Isa 43:25

c Yoh 5:6-9

d Mt 9:9
Mk 2:14

e Mt 9:10-13
Mk 2:15-17

Safu ya 2

a Lu 15:1, 2

b Isa 53:4
Mt 9:12
Mk 2:17

c Mt 9:13
1Ti 1:15

d Mt 9:14,15
Mk 2:18-20
Lu 7:34

e Mt 22:2
2Ko 11:2
Ufu 19:7

f Yoh 16:19, 20

g Mt 9:16, 17
Mk 2:21, 22

ndishi wao wakaanza kuwalamikia wanafunzi wake, wakisema: “Kwa nini mnakula na kunywa pamoja na waku-sanya kodi na watenda dhambi?”^a

31 Yesu akawajibu: “Watu wenyewe afya hawahitaji daktari, lakini wagonjwa wanamhitaji.”^b

32 Sikuja kuwaita waadilifu, bali kuwahimiza watenda dhambi watubu.”^c

33 Wakamwambia: “Wanafunzi wa Yohana hufunga mara nyingi na kutoa dua, na pia wanafunzi wa Mafarisayo, lakini wanafunzi wako hula na kunywa.”^d

34 Yesu akawaambia: “Hamwezi kuwafanya rafiki za bwana harusi wafunge bwana harusi akiwa pamoja nao, sivyo? **35** Lakini siku zitakuja ambapo kwa kweli bwana harusi^e ataondolewa kwao; ndipo watakapofunga siku hizo.”^f

36 Pia, akawapa mfano: “Hakuna mtu anayekata kiraka cha vazi jipya la nje na kukishona kwenye vazi la zamani. Akifanya hivyo, kiraka kipya hurarua vazi la zamani na kiraka kipya hakilingani na vazi la zamani.”^g

37 Pia, hakuna mtu anayeweka divai mpya katika viriba vya divai vilivyochakaa. Akifanya hivyo, divai mpya itavipasua viriba, nayo itamwagika na viriba vitaharibika. **38** Lakini divai mpya lazima iwekwe katika viriba vipya vya divai. **39** Mtu anapokunywa divai ya zamani hapendi divai mpya, kwa maana husema, ‘Ile ya zamani ndiyo nzuri.’”

6 Siku moja ya Sabato Yesu alipokuwa akipita katika mashamba ya nafaka, wanafunzi wake walikuwa wakivunja na kula masuke ya nafa-

5:29 *Au “walikuwa wameketi mezani.”

ka,^a wakiyapukusa kwa miko-no yao.^b **2** Ndipo baadhi ya Mafarisayo wakauliza: “Kwa nini mnafanya jambo lisilo halali siku ya Sabato?”^c **3** Lakini Yesu akawajibu: “Je, hamjasma alilofanya Daudi wakati yeye na wanaume waliokuwa pamoja naye walipohisi njaa?^d **4** Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu akapokea mikate ya toleo,* akala na pia akawapa wanaume waliokuwa pamoja naye, mikate ambayo si halali kwa yeyote kula ila makuhani tu?”^e **5** Kisha akawaambia: “Mwana wa binadamu ndiye Bwana wa Sabato.”^f

6 Siku nyingine ya Sabato^g aliingia katika sinagoga, akaanza kufundisha. Kulikuwa na mtu aliyepooza mkono wa kulia.^h **7** Waandishi na Mafarisayo walikuwa wakimwambia Yesu kwa makini ili waone kama angeponya katika siku ya Sabato, ili wapat sababu ya kumshtaki. **8** Hata hivyo, alijua mawazo yao,ⁱ basi akamwambia yule mtu aliyepooza mkono: “Inuka usimame hapa katikati.” Naye akainuka na kusimama hapo. **9** Kisha Yesu akawauliza: “Je, ni halali kufanya mema au kufanya mabaya siku ya Sabato, kuokoa uhai* au kuuangamiza?”^j **10** Baada ya kuwatazama wote waliokuwapo, Yesu akamwambia mtu huyo: “Nyoocha mkono wako.” Akaunyoosha, nao ukapona. **11** Lakini wakakasirika sana, wakaanza kushauriana kuhusu jambo ambalo wangemte-ndea Yesu.

12 Siku moja, Yesu alienda

6:4 *Au “mikate ya wonyesho.” 6:9 *Au “nafsi.”

SURA YA 6

a Kum 23:25

b Mt 12:1-8
Mk 2:23-28

c Kut 20:9,10
Kum 5:13,14
Yoh 5:9,10

d 1Sa 21:1-6

e Law 24:5-9

f Mt 12:8
Mk 2:27,28

g Lu 13:14
Yoh 9:16

h Mt 12:9-14
Mk 3:1-6

i Lu 5:22
Yoh 2:24,25

j Mt 12:11
Mk 3:4
Yoh 7:23

Safu ya 2

a Mt 6:6
Mk 3:13

b Mt 14:23

c Mt 10:2-4
Mk 3:14-19
Mdo 1:13

d Yoh 14:8

e Yoh 11:16

f Mk 5:30

g Mt 5:2,3
Yak 2:5

h Zb 107:9
Isa 55:1
Yer 31:25
Mt 5:6

i Isa 61:3
Ufu 21:4

j Mt 5:10,11
Yoh 17:14
1Pe 3:14

k Yoh 16:2

mlimani kusali,^a naye akasali kwa Mungu usiku wote.^b **13** Kulipokucha akawaita wanafunzi wake na kuchagua 12 kati yao, ambao pia aliwaita mitume:^c **14** Simoni, ambaye pia alimwita jina Petro, Andrea ndugu yake, Yakobo, Yohana, Filipo,^d Bartholomayo, **15** Mathayo, Tomasi,^e Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni anayeitwa “mwenye bidii,” **16** Yuda mwana wa Yakobo, na Yuda Iskariote, aliyegeuka kuwa msaliti.

17 Yesu akashuka pamoja nao akasimama mahali tambarare, na kulikuwa na umati mkubwa wa wanafunzi wake, na umati mkubwa wa watu kutoka Yudea yote na Yerusalemu na eneo la pwani la Tiro na Sidoni, waliokuja kumsikiliza na kuponywa magonjwa. **18** Hata aliwaponya wale waliosumbuliwa na roho waovu. **19** Umati wote ulikuwa ukijaribu kungusa, kwa sababu nguvu zilikuwa ziki-**mtoka^f** na kuwaponya wote.

20 Akainua macho na kuwatazama wanafunzi wake na kusema:

“Wenye furaha ni ninyi maskini, kwa sababu Ufalme wa Mungu ni wenu.^g

21 “Wenye furaha ni ninyi mlio na njaa sasa, kwa sababu mtashiba.^h

“Wenye furaha ni ninyi mnaolia sasa, kwa sababu mtacheka.ⁱ

22 “Wenye furaha ni ninyi watu wanapowachukia,^j wanapowatenga,^k wanapowashutumu, na kuwachafulia jina* kwa ajili ya Mwana wa binadamu. **23** Siku hiyo shangilieni na

6:22 *Au “kukataa jina lenu.”

kuruka kwa shangwe, kwa maana tazama! thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa kuwa mababu zao waliwatendea manabii mambo hayohayo.^a

24 “Lakini ole wenu ninyi matajiri,^b kwa sababu mnapata faraja yenu kikamili.^c

25 “Ole wenu ninyi mlioshiba sasa, kwa sababu mtakuwa na njaa.

“Ole wenu ninyi mnaocheka sasa, kwa sababu mtaomboleza na kulia.^d

26 “Ole wenu watu wote wanapowasifu,^e kwa maana hivyo ndivyo mababu zao walivyowatendea manabii wa uwongo.

27 “Lakini ninawaambia ninyi mnaosikiliza: Endeleeni kuwapenda adui zenu na kuwatendea mema wale wanaowachukia,^f **28** kuwabariki wale wanaowalaani, na kusali kwa ajili ya wale wanaowatukana.^g **29** Anayekupiga kwenye shavu moja, mgeuzie pia shavu lingine; na anayechukua vazi lako la nje, usimzuilie hata vazi la ndani.^h **30** Mpe kila mtu anayekuomba,ⁱ na yule anayechukua vitu vyako, usimwombe akurudishie.

31 “Pia, kama vile mnavyotaka watu wawatendee ninyi, watendeeni vivyo hivyo.^j

32 “Mkiwapenda wale wanaowapenda, mnapata faida gani? Kwa maana hata watenda dhambi huwapenda wale wanaowapenda.^k **33** Na mkiwatendea mema wale wanaowatendea mema, mnapata faida gani? Hata watenda dhambi hufanya vivyo hivyo. **34** Pia, mkiwakopesha* wale tu ambao mnamtambuni wata-

6:34 *Yaani, mkiwakopesha bila faida.

SURA YA 6

a 2Nya 36:16
Mt 5:12
Lu 11:47
Mdo 7:52

b Yak 5:1

c Mt 6:2

d Isa 65:13

e Yak 4:4
1Yo 4:5

f Kut 23:4
Met 25:21
Mt 5:44
Ro 12:20

g Mdo 7:59, 60
Ro 12:14

h Mt 5:39, 40
1Ko 6:7

i Kum 15:7, 8
Met 3:27
Met 21:26
Mt 5:42

j Mt 7:12

k Mt 5:46, 47

Safu ya 2

a Law 25:35, 36
Kum 15:7, 8
Mt 5:42

b Kut 22:25
Law 25:37
Kum 23:20
Zb 37:25, 26

c Mt 5:45
Mdo 14:17

d Mt 5:48
Efe 5:1, 2
Yak 2:13

e Mt 7:1, 2
Ro 14:10

f Mt 6:14
Mk 11:25

g Met 19:17

h Mt 15:14

i Mt 7:3-5

walipa, mnapata faida gani?^a Hata watenda dhambi huwakopesha watenda dhambi ili warudishiwe kiasi kilekile.

35 Badala yake, endeleeni kuwapenda adui zenu, kutenda mema, na kukopesha bila kutumaini kurudishiwa;^b nanyi mtapata thawabu kubwa, na mtakuwa wana wa Aliye Juu Zaidi, kwa sababu yeye huwaonyesha fadhili hata watu wasio na shukrani na waovu.^c

36 Endeleeni kuwa wenye rehema, kama Baba yenu alivyo mwenye rehema.^d

37 “Zaidi ya hayo, acheni kuhukumu, nanyi hamtahukumiwa kamwe;^e na acheni kulaumu, nanyi hamtalumiwa kamwe. Endeleeni kusa-mehe, * nanyi mtasamehewa.^f

38 Muwe na mazoea ya kuwapa watu, nanyi mtapewa.^g Watawamwagia kwenye mfuko wa nguo zenu kipimo kizuri, kilichoshindiliwa, kilichotiki-swa, na kufurika. Kwa maana kwa kipimo mnachowapimia watu, ndicho watawachowapimia.”

39 Kisha akawaambia mfanoo huu: “Je, kipofu anaweza kumwongoza kipofu mwenzake? Wote watatumbukia shimoni, sivyo?^h **40** Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, lakini kila mtu aliyefundishwa kikamili atakuwa kama mwalimu wake. **41** Basi, kwa nini unautazama unyasi ulio katika jicho la ndugu yako lakini hutambui boriti lililo katika jicho lako mwenyewe?ⁱ **42** Unawezaje kumwambia ndugu yako, ‘Ndugu, niruhusu niutoe unyasi ulio katika jicho lako,’ waka-

6:37 *Au “kuachilia.” #Au “mtaachiliwa.”

ti wewe mwenyewe huoni boriti lililo katika jicho lako? Mnafiki! Kwanza toa boriti katika jicho lako, kisha utaona vizuri jinsi ya kuutoa unyasi ulio katika jicho la ndugu yako.

43 "Kwa maana hakuna mti mzuri unaozaa matunda yaliyooza, wala hakuna mti uliooza unaozaa matunda mazuri.^a

44 Kwa maana kila mti hujulikana kwa matunda yake.^b Kwa mfano, watu hawachumi tini kwenye miiba, wala kukata zabibu kwenye miti ya miiba.

45 Mtu mwema hutoa mambo mema kwenye hazina njema ya moyo wake, lakini mtu mwovu hutoa maovu kwenye hazina yake mbovu; kwa maana kinywa husema mambo yaliyojaa moyoni.^c

46 "Basi kwa nini mnaniita 'Bwana! Bwana!' lakini hamfanyi mambo ninayosema?^d

47 Nitawaonyesha jinsi alivyo kila mtu anayekuja kwangu na kusikia maneno yangu na kisha kuyatenda:^e **48** Ni kama mtu aliyejenga nyumba kwa kuchimba kina kirefu na kuweka msingi kwenye mwamba. Baadaye, mafuriko yalipotokea, mto ukaipiga nyumba hiyo, lakini haikutikisika, kwa sababu ilikuwa imejengwa vizuri.^f **49** Kwa upande mwingine, yule anayesikia na hatendi,^g ni kama mtu aliyejenga nyumba juu ya udongo, bila msingi. Mto ukaipiga nyumba hiyo, nayo ikaporomoka mara moja, na kuharibika kabisa."

7 Alipomaliza kuzungumza na watu, akaingia Kaper-naumu. **2** Ofisa fulani wa jeshi alikuwa na mtumwa aliyependa sana, na ambaye

SURA YA 6

a Mt 7:16-18

b Mt 12:33

c Mt 12:34, 35

d Mt 7:21
Lu 13:24
Ro 2:13
Yak 1:22

e Mt 7:24-27

f Zb 125:1

g Yak 1:23, 24

Safu ya 2

SURA YA 7

a Mt 8:5, 6

b Mt 8:8, 9

c Mt 8:10

d Mt 8:13

e Ifa 17:17
Lu 8:41, 42

alikuwa mgonjwa sana karibu kufa.^a **3** Aliposikia kuhusu Yesu, akawatuma wazee fulani wa Wayahudi wamwombe Yesu aje kumponya mtumwa wake.

4 Walipofika kwa Yesu wamsihi sana wakisema: "Mfanyie jambo hilo, anastahili **5** kwa maana analipenda taifa letu na yeye ndiye aliyetujengea sinagogi." **6** Basi Yesu akaenda pamoja nao. Alipokaribia nyumba hiyo, yule ofisa wa jeshi alikuwa tayari amewatuma rafiki zake wamwambie: "Bwana, usijisumbue, kwa maana mimi sistahili uingie ndani ya nyumba yangu.^b

7 Ndiyo sababu niliona sistahili kuja kwako. Lakini sema tu neno, na mtumishi wangu atapona. **8** Kwa maana mimi pia niko chini ya mamlaka, na nina wanajeshi walio chini yangu, nami humwambia mmoja, 'Nenda!' naye huenda, na mwingine, 'Njoo!' naye huja, na mtumwa wangu, 'Fanya hili!' naye hulifanya."

9 Yesu aliposikia maneno hayo alishangazwa naye, akaugeukia umati uliokuwa ukimfuata na kusema: "Ninawaambia, hata katika Israeli sijaona imani kubwa kama hii."^c **10** Na wale waliokuwa wametumwa waliporudi nyumbani, wakamkuta yule mtumwa amepona.^d

11 Muda mfupi baadaye, Yesu akasafiri pamoja na wanafunzi wake na umati mkubwa kwenda jiji linaloitwa Naini. **12** Alipokaribia lango la jiji, tazama! kulikuwa na watu waliokuwa wamebeba maiti wakiipeleka nje, yule aliyekufa alikuwa mwana pekee,^e na mama yake^e alikuwa mjane.

7:12 * Tnn., "mwana mzaliwa pekee."

Watu wengi kutoka jijini walikuwa pamoja na yule mwanamke. **13** Bwana alipomwona yule mjane akamsikitikia^a na kumwambia: "Acha kulia."^b

14 Akakaribia na kuligusa jeneza, * nao wale waliolibeba wakasimama. Akasema: "Kijana, ninakuambia, inuka!"^c

15 Yule mfu akaketi akaanza kuongea, naye Yesu akamkabidhi kwa mama yake.^d **16** Basi wote wakaogopa, wakaanza kumtukuza Mungu wakisema: "Nabii mkuu ameinuliwa kati yetu,"^e na, "Mungu amewakumbuka watu wake."^f **17** Habari hizo kumhusu Yesu zikaenea katika Yudea yote na maeeneo jirani.

18 Basi wanafunzi wa Yohana wakamjulisha mambo hayo yote.^g **19** Ndipo Yohana akawaaita wawili kati ya wanafunzi wake akawatuma kwa Bwana wamuulize: "Je, wewe ndiye Yule Anayekuja,^h au tumtarajie mwingine?" **20** Walipofika kwa Yesu wakamwambia: "Yohana Mbatizaji alitutuma kwako tukuulize: 'Je, wewe ndiye Yule Anayekuja au tumtarajie mwingine?'"

21 Wakati wahuohuo, Yesu akawaponya watu wenye magonjwa,ⁱ maradhi hatari, na wenye roho waovu, na pia akawapa vipofu wengi zawadi ya kuona. **22** Kisha akawajibu: "Nendeni mkamwambie Yohana mambo mliyoona na kusikia. Vipofu wanaona,^j viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia,^k wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.^l **23** Mwenye furaha

7:14 *Au "machela ya kubebea maiti."

SURA YA 7

a Ebr 4:15

b Lu 8:52
Yoh 11:33

c 1Fa 17:21, 22
Lu 8:52-54
Yoh 11:43
Mdo 9:40

d 1Fa 17:23
2Fa 4:36

e Kum 18:15
Yoh 4:19
Yoh 6:14
Yoh 7:40

f Lu 1:68

g Mt 11:2-6

h Zb 40:7
Zb 118:26
Zek 9:9
Mt 3:11

i Isa 53:4

j Isa 42:7

k Isa 29:18
Isa 35:5, 6

l Isa 61:1
Lu 4:18
Yak 2:5

Safu ya 2

a Isa 8:14
Lu 2:34
Yoh 6:66

b Mt 11:7-11

c Mk 1:6

d Mk 1:2
Lu 1:67, 76

e Isa 40:3
Mal 3:1
Lu 1:16, 17
Yoh 1:23

f Mt 11:11

g Mt 3:5, 6
Lu 3:12

h Mdo 13:46
Ro 10:2, 3

i Mt 11:16-19

ni mtu ambaye hapati ndani yangu sababu ya kukwaza."^a

24 Wajumbe wa Yohana walipoondoka, Yesu akaanza kuuambia umati kumhusu Yohana: "Mlienda nyikani kuona nini? Tete likitikiswa na upepo?"^b **25** Basi, mlienda kuona nini? Mtu aliyevaa mavazi laini?^{*c} Kwa maana wale wanaovaa mavazi maridadi na kuishi maisha ya anasa hukaa katika nyumba za kifalme.

26 Basi kwa kweli, mlienda kuona nini? Nabii? Ndiyo, ninawaambia, mtu aliye zaidi ya nabii.^d **27** Huyu ndiye ambaye imeandikwa hivi kumhusu, 'Tazama! Nina mtuma mjumbe wangu mbele yako,* ili akutayarishie njia mbele yako.'^e **28** Ninawaambia, kati ya wale waliozalitwa na wanawake hakuna aliye mkuu kuliko Yohana, lakini mtu mdogo zaidi katika Ufalme wa Mungu, ni mkuu kuliko Yohana."^f **29** (Watu wote na wakusanya kodi waliposikia jambo hilo, wakamtangaza Mungu kuwa mwadilifu, kwa sababu walikuwa wamebatizwa kwa ubatizo wa Yohana.^g

30 Lakini Mafarisayo na wale wenye ujuzi wa Sheria walilipuuza shauri la* Mungu,^h kwa sababu hawakuwa wamebatizwa na Yohana.)

31 "Basi, nitawalinganisha watu wa kizazi hiki na nani, wanafanana na nani?"ⁱ

32 Wao ni kama watoto walioketi sokoni ambao wanaambiana kwa sauti kubwa, wakisema: 'Tuliwapigia filimbi, lakini hamkucheza dansi;

7:25 *Au "mavazi bora?" 7:27 *Tnn., "mbele ya uo wako." 7:30 *Au "mwongozo wa."

tuliomboleza, lakini hamkulia.' **33** Vivyo hivyo, Yohana Mbatizaji hakuja akila mka-te wala kunywa divai,^a lakini mnasema: 'Ana roho mwovu.' **34** Mwana wa binadamu amekuja akila na kunywa, lakini mnasema: 'Tazama! yeye ni mlafi na mwenye mazoea ya kunywa divai, rafiki ya waku-sanya kodi na watenda dhambi!'^b **35** Hata hivyo, heki-ma huthibitishwa* kuwa ye-nye uadilifu kupitia watoto wake wote."^c

36 Mmoja wa Mafarisayo alikuwa akimwomba Yesu ale pamoja naye. Basi akaenda ka-tika nyumba ya Farisayo huyo na akaketi mezani. **37** Taza-ma! mwanamke aliyejulika-na jijini kuwa mtenda dhambi akapata habari kwamba Yesu alikuwa akila* katika nyumba ya Farisayo, naye akaja na chupa ya alabasta yenye ma-futa ya marashi.^d **38** Akaketi miguuni pa Yesu, akalia na ku-lowesha miguu yake kwa ma-chozi na kuifuta kwa nywele za kichwa chake. Pia, akaibu-su kwa wororo miguu ya Yesu na kuipaka mafuta ya mara-shi. **39** Alipoona hivyo, yule Farisayo aliyemwalika akajia-ambia: "Kama kweli mtu huyu angekuwa nabii, angejua ni nani na ni mwanamke wa aina gani anayemgusa, kwamba ni mtenda dhambi?"^e **40** La-kini Yesu akamwambia: "Si-moni, ninataka kukuambia ja-mbo." Akasema: "Sema, mwa-limu!"

41 "Mtu fulani aliwakope-sha watu wawili pesa, mmoja

SURA YA 7

a Hes 6:2, 3
Mt 3:4
Lu 1:13, 15

b Mt 11:19
Lu 5:30

c Yoh 10:37, 38

d Mt 26:6, 7
Mk 14:3
Yoh 12:3

e Lu 15:2

Safu ya 2

a Zb 32:1
Zb 51:1
Zb 103:2, 3
Isa 1:18
Isa 43:25
Isa 44:22

b Mt 9:2
Mk 2:5

c Mk 2:7
Lu 5:21

d Mt 9:22
Lu 8:48

SURA YA 8

e Mt 9:35
Lu 4:43

alikuwa na deni la dinari* 500, na mwingine 50. **42** Walipo-shindwa kumlipa, akawa-samehe kwa hiari wote wa-wili. Kwa hiyo, ni nani kati yao atakayempenda zai-di?" **43** Simoni akajibu: "Na-dhani ni yule aliyesamehewa zaidi." Akamwambia: "Ume-jibu vizuri." **44** Ndipo aka-mgeukia yule mwanamke na kumwambia Simoni: "Una-mwona mwanamke huyu? Ni-liingia katika nyumba yako; hukunipa maji ya kuosha miguu yangu. Lakini mwanamke huyu aliiosha miguu yangu kwa machozi yake na kuifuta kwa nywele zake. **45** Wewe hukunibusu, lakini mwanamke huyu hajaacha kui-busu miguu yangu kwa woro-ro tangu nilipoingia. **46** Hu-kunipaka mafuta kichwani, la-kini mwanamke huyu ameipa-ka miguu yangu mafuta yenye marashi. **47** Kwa hiyo, nina-kuambia ingawa dhambi zake ni nyingi,* amesamehewa,^a kwa sababu amependa sana. Lakini anayesamehewa kido-go, hupenda kidogo." **48** Ndi-po akamwambia mwanamke huyo: "Umesamehewa dha-mbi zako."^b **49** Wale walioke-ti mezani pamoja naye wakaa-nza kuulizana: "Mtu huyu ni nani ambaye hata anasame-he dhambi?"^c **50** Lakini aka-mwambia yule mwanamke: "Imani yako imekuokoa;^d nenda kwa amani."

8 Muda mfupi baadaye Yesu akasafiri kutoka jiji mpa-ka jiji na kijiji mpaka kijiji, akihubiri na kutangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu.^e

7:41 * Angalia Nyongeza B14. 7:47 * Au "kubwa."

7:35 * Au "hutetewa." ^a Au "kupitia ma-tokeo yake." 7:37 * Au "alikuwa ameketi mezani."

Wale 12 walikuwa pamoja naye, **2** na pia wanawake fulani waliotolewa roho waovu na kuponywa magonjwa, yaani: Maria aitwaye Magdalene, ambaye alitolewa roho waovu saba; **3** Yoana^a mke wa Kuza, msimamizi wa nyumba ya Herode; Susana; na wanawake wengine wengi waliokuwa wakiwahudumia kwa mali zao.^b

4 Umati mkubwa na pia watu waliokuja kutoka majiji mbalimbali walipokusanyika, Yesu akawaambia mfano huu:^c **5** "Mpandaji alienda kupanda mbegu. Alipokuwa akipanda, mbegu fulani zikaanguka kando ya barabara zikakanyagwa-kanyagwa, na ndege wa angani wakazila.^d **6** Nyingine zikaanguka kwenye mwamba, na baada ya kuchipuka, zikakauka kwa kukosa maji.^e **7** Nyingine zikaanguka kwenye miiba, nayo miiba ikakua pamoja nazo na kuzisonga.^f **8** Lakini nyingine zikaanguka kwenye udongo mzuri, zikachipuka na kuzaa matunda mara 100 zaidi."^g Baada ya kusema hayo, akasema kwa sauti kubwa: "Yule aliye na masikio ya kusikiliza, na asikilize."^h

9 Lakini wanafunzi wake wakamuuliza maana ya mfano huo.ⁱ **10** Akawaambia: "Ninyi mmepewa uwezo wa kuelewa siri takatifu za Ufalme wa Mungu, lakini ninazungumza na wale wengine kwa kifano,^j ili ingawa wanatazama, watazame lakini wasione, na ingawa wanasikia, wasielewe.^k **11** Basi mfano huo unamaanisha hivi: Mbegu ni neno la Mungu.^l **12** Mbegu zilizoanguka kando ya ba-

SURA YA 8

a Lu 24:9, 10

b Mt 27:55
Mk 15:40, 41c Mt 13:1-3
Mk 4:1, 2d Mt 13:3-9
Mk 4:3-9
Lu 8:12

e Lu 8:13

f Lu 8:14

g Lu 8:15

h Mt 11:15
Mt 13:9
Mk 4:9i Mt 13:10
Mk 4:10j Zb 78:2
Mt 13:34, 35
Mk 4:34k Isa 6:9, 10
Mt 13:11, 13
Mk 4:11, 12l Mt 13:18-23
Mk 4:14-20

Safu ya 2

a Mt 13:19
Mk 4:15
2Ko 4:3, 4b Mt 13:20, 21
Mk 4:16, 17c Mt 19:23
1Ti 6:9

d 2Ti 4:10

e Mt 13:22
Mk 4:18, 19

f Mdo 16:14

g Mt 13:23
Mk 4:20
Ebr 10:36h Mt 5:15
Mk 4:21
Lu 11:33
Flp 2:15i Mt 10:26
Mk 4:22
Lu 12:2

j Mt 25:23

k Mt 13:12
Mt 25:29
Mk 4:24, 25
Lu 19:26l Mt 13:55
Yoh 7:5
Mdo 1:14m Mt 12:46, 47
Mk 3:31, 32

rabara ni wale ambao husikia, kisha Ibilisi huja na kuliondoa lile neno mioyoni mwao ili wasiamini na kuokolewa.^a

13 Mbegu zilizoanguka kwenye mwamba ni wale ambao wanapolisikia neno hulipokea kwa shangwe, lakini hawana mizizi. Wanaamini kwa muda, hata hivyo wanapojari-biwa wanaanguka.^b **14** Mbegu zilizoanguka kwenye miiba, ni wale ambao wamesikia, lakini wanakengeushwa na mahangaiko, utajiri,^c na raha za maisha.^d Wao husongwa kabisa na hawakomai.^e **15** Nazo mbegu zilizoanguka kwenye udongo mzuri, ni wale wenye moyo mzuri na mwe-ma,^f ambao baada ya kulisikia neno hulihifadhi na kuzaa matunda kwa uvumilivu.^g

16 "Hakuna mtu anayewasha taa na kuifunika kwa chombo au kuiweka chini ya kitanda, bali huiweka kwenye kinara cha taa, ili iwaangazie wale wanaoingia.^h **17** Kwa maana hakuna jambo lolote lililofichwa ambalo halitafunuliwa, wala jambo lolote lililofunikwa kwa uangalifu ambalo halitajulikana na kuwa wazi.ⁱ

18 Kwa hiyo, kazieni uangalifu jinsi mnavyosikiliza, kwa maana yule aliye na kitu atao-ngezewa,^j lakini yule asiye na kitu, hata kile anachowazia kwamba anacho kitachukuliwa."^k

19 Sasa mama yake na ndugu zake^l wakaja, lakini hawakuweza kumfikia Yesu kwa sababu ya umati.^m **20** Basi akaambiwa: "Mama yako na ndugu zako wamesimama nje, wanataka kukuona."ⁿ **21** Akawajibu: "Mama yangu na ndu-

gu zangu ni hawa wanaosikia neno la Mungu na kulitenda.”^a

22 Siku moja, Yesu na wanafunzi wake walipanda mashua, naye akawaambia: “Tuvuke twende ng’ambo ya ziwa.” Basi wakaondoka.^b **23** Walipokuka wakisafiri akalala usingizi. Dhoruba kali ya upepo ikatokea kwenye ziwa na mashua yao ikaanza kujaa maji ikakaribia kuzama.^c **24** Basi wakaenda kumwamsha na kusema: “Mwalimu, Mwalimu, tuko karibu kuangamia!” Ndipo akasimama, akaukemea upepo na mawimbi ya maji, nayo dhoruba ikatulia, kukawa shwari.^d **25** Kisha akawauliza: “Kwa nini hamna imani?” Lakini wakaogopa na kushangaa, wakaambiana: “Kwa kweli, mtu huyu ni nani? Kwa maana anaamuru upepo na maji, navyo vina-
mtii.”^e

26 Wakafika pwani ya eneo la Wagerasene,^f lililo ng’ambo ya Galilaya. **27** Yesu alipotoka kwenye mashua akakutana na mwanamume fulani kutoka jijini aliyekuwa na roho mwovu. Hakuwa amevaa nguo kwa muda mrefu, na hakuwa akiishi katika nyumba bali aliishi makaburini.^{*g} **28** Alipomwona Yesu, akapaza kilio na kuanguka chini mbele yake, akasema kwa sauti kubwa: “Kwa nini unanisumbua, Yesu, Mwana wa Mungu Aliye Juu Zaidi? Ninakuomba, usinitese.”^h **29** (Kwa maana Yesu alikuwa akimwagiza huyo roho mwovu amtoke. Kwa sababu alikuwa amemshika mtu huyo mara nyingi,^{*i} naye ali-

SURA YA 8

a Mt 12:48-50
Mk 3:33-35
Yoh 15:14

b Mt 8:18, 23
Mk 4:35, 36

c Mt 8:24-27
Mk 4:37-41

d Zb 89:9

e Mt 8:27
Mk 4:41

f Mk 5:1

g Mt 8:28, 29
Mk 5:2-10

h Mk 1:23, 24

i Mk 9:20, 21

Safu ya 2

a Ufu 20:2, 3

b Law 11:7, 8
Kum 14:8

c Mt 8:30-34
Mk 5:11-17

fungwa mara kwa mara kwa minyororo na pingu na kuwekwa chini ya ulinzi, lakini alivunja vifungo hivyo na yule roho mwovu akampeleka mahali pasipo na watu.) **30** Yesu akamuuliza: “Jina lako ni nani?” Akajibu: “Kikosi,” kwa sababu alikuwa ameingiwa na roho wengi waovu. **31** Nao wakaendelea kumsihi asiwaamuru waende katika shimo refu lisilo na mwisho.^{*a} **32** Sasa kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe^b waliokuwa wakila mlimani, basi wakamsihi awaruhusu waingie ndani ya nguruwe hao, naye akawaruhusu.^c **33** Ndipo wale roho waovu wakamtoka mtu huyo na kuingia ndani ya wale nguruwe, kisha lile kundi likati-mua mbio, likaruka poromoko,^{*d} likazama ndani ya ziwa na kufa maji. **34** Wachungaji walipoona kilichotokea, wakakimbia na kupeleka habari hizo jijini na mashambani.

35 Ndipo watu wakaenda kuona kilichotokea. Wakamjia Yesu na kumkuta yule mtu aliyetokwa na roho waovu ameketi miguuni pa Yesu, akiwa amevaa nguo na akiwa na akili timamu, nao wakaogopa. **36** Wale walioona jambo hilo wakawasimulia jinsi yule mtu aliyekuwa na roho waovu alivyoponywa. **37** Kisha watu wengi kutoka nchi ya Wagerasene wakamwomba Yesu aondoke, kwa sababu walikuwa wameogopa sana. Ndipo akapanda mashua ili aondoke. **38** Hata hivyo, yule mwanamume aliyetokwa na

8:27 *Au “makaburi ya ukumbusho.”

8:29 *Au labda, “alikuwa amemshika kwa muda mrefu.”

8:31 *Au “abiso.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 8:33 *Au “ukingo wenye mteremko mkali.”

roho waovu akaendelea kumsihi aende pamoja naye, lakini Yesu hakumruhusu, akamwambia:^a **39** "Rudi nyumbani na uendeleo kusimulia mambo ambayo Mungu amekutendea." Basi akarudi, akitangaza katika jiji lote mambo ambayo Yesu alimtendea.

40 Yesu aliporudi, umati ukampokea kwa fadhili, kwa maana wote walikuwa wakimtarajia.^b **41** Lakini tazama! mwanamume anayeitwa Yairo akaja, alikuwa ofisa msimamizi wa sinagogi. Akajiangusha miguuni pa Yesu akaanza kumsihi aende nyumbani kwake.^c **42** kwa sababu binti yake wa pekee,* mwenye umri wa miaka 12 hivi, alikuwa karibu kufa.

Yesu alipokuwa akienda umati ukamsonga. **43** Kulikuwa na mwanamke aliye kuwa na mtiririko wa damu^d kwa miaka 12, na hakuwa amepata mtu wa kumponya.^e **44** Akaja kutoka nyuma na kugusa upindo wa vazi lake la nje,^f na mara moja akacha kutokwa damu. **45** Ndipo Yesu akauliza: "Ni nani aliyenigusa?" Wote walipokuwa wakikana, Petro akasema: "Mwalimu, umati ume-kuzunguka na kukusonga."^g **46** Lakini Yesu akasema: "Mtu fulani amenigusa, kwa maana ninajua nguvu^h zime-nitoka." **47** Yule mwanamke alipoona kwamba hakuepu-ka kutambuliwa, akaja akitetemeka na kuanguka chini mbele yake, akaeleza mbele ya watu wote sababu iliyomfanya amguse na jinsi alivyoponywa mara moja. **48** Lakini Yesu akamwambia: "Binti ya-

8:42 *Tnn., "mzaliwa pekee."

SURA YA 8

a Mk 5:18-20

b Mk 5:21

c Mt 9:18, 19
Mk 5:22-24

d Law 15:25

e Mt 9:20-22
Mk 5:25-29

f Hes 15:38, 39

g Mk 5:30-34

h Lu 5:17

Safu ya 2

a Mt 9:22
Lu 7:50

b Mk 5:35-37

c Yoh 11:25
Ro 4:17

d Lu 7:12, 13

e Mt 9:23-26
Mk 5:38-43
Yoh 11:11
Mdo 7:60
Mdo 13:36

f Mk 5:41
Lu 7:14
Yoh 11:43

g Mwa 2:7
Mhu 3:19
Isa 42:5

h Mk 5:42

i Mk 7:35, 36

SURA YA 9

j Mk 6:7

k Mt 10:1

l Mt 10:9, 10
Mk 6:8, 9
Lu 10:4

ngu, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani."^a

49 Alipokuwa bado akizungumza, mwakilishi wa yule ofisa msimamizi wa sinagogi akaja na kusema: "Binti yako amekufa, usiendeleo kumsumbua Mwalimu."^b **50** Yesu aliposikia hilo akamwambia: "Usiogope, uwe tu na imani, naye ataokolewa."^c **51** Alipofika kwenye nyumba hiyo, hakumruhusu yeyote angie pamoja naye ila Petro, Yohana, Yakobo, na wazazi wa yule msichana. **52** Lakini watu wote walikuwa wakilia na kuji-pigapiga kwa huzuni kwa sababu ya yule msichana. Basi akawaambia: "Acheni kulia,^d kwa maana hajafa bali amelala usingizi."^e **53** Ndipo wakaa-nza kumcheka kwa dharau, kwa sababu walijua amekufa. **54** Lakini akamshika mkono na kumwita: "Mtoto, inuka!"^f **55** Roho^g yake ikarudi* naye akasimama mara moja,^h kisha Yesu akaagiza apewe chakula. **56** Basi, wazazi wake wakafurahi sana, lakini Yesu akawaagiza wasimwambie mtu yeyote kilichotukia.ⁱ

9 Ndipo akawaita pamoja wale 12, akawapa nguvu na mamlaka ya kufukuza roho wote waovu^j na kuponya magonjwa.^k **2** Kisha akawatuma kuhubiri kuhusu Ufalme wa Mungu na kuponya, **3** akawaambia: "Msibe-be chochote kwa ajili ya safari, wala fimbo wala mfuko wa chakula wala mkate wala pesa;* wala msiwe na mavazi mawili."^l **4** Lakini mtaka-poingia katika nyumba yoyo-

8:55 *Au "nguvu za uhai zikarudi." 9:3 *Tnn., "fedha." ^aAu "vazi la ziada."

te, kaeni humo mpaka mtaka-poondoka huko.^a **5** Popote ambapo watu hawatawakaribisha, mnapotoka katika jiji hilo kung'uteni mavumvi yalio kwenye miguu yenu ili uwe ushahidi dhidi yao.”^b **6** Kisha wakaenda katika eneo hilo kutoka kijiji mpaka kijiji, wakita-ngaza habari njema na kuponya wagonjwa kila mahali.^c

7 Basi Herode* mtawala wa wilaya[#] aliposikia kuhusu mambo yaliyokuwa yakitukia, akashikwa na wasiwasi sana kwa sababu watu walikuwa wakisema Yohana alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu,^d **8** lakini wengine walikuwa wakisema Eliya alikuwa ametokea, na wengine mmoja wa manabii wa kale alikuwa amefufuliwa.^e **9** Herode akasema: “Yohana nilimkata kichwa.^f Basi, ni nani huyu ninayesikia habari hizi kumhusu?” Kwa hiyo alitamani kumwona.^g

10 Mitume waliporudi, wakamsimulia Yesu mambo yote waliyokuwa wamefanya.^h Ndi-po akaondoka nao na kwenenda faraghani katika jiji linaloitwa Bethsaida.ⁱ **11** Lakini umati ulipojua, ukamfuata. Yesu akawapokea kwa fadhili na kuanza kuwaambia kuhusu Ufalme wa Mungu, naye akawaponya wale waliohitaji kuponywa.^j **12** Ilipokaribia jioni, wale 12 wakaja na kumwambia Yesu: “Uambie umati uondoke, waende vijijini na mashambani ili wakatafute chakula na mahali pa kuala, kwa sababu mahali hapa hapana watu.”^k **13** Lakini

9:7 * Yaani, Herode Antipa. Angalia Kamusi, uku. 2012. “Tnn., “tetraki.”

SURA YA 9

a Mt 10:11
Mk 6:10
Lu 10:5, 7

b Mt 10:14
Mk 6:11
Lu 10:10, 11
Mdo 13:50, 51

c Mt 11:1
Mk 6:12, 13

d Mt 14:1, 2
Mk 6:14-16

e Mk 8:27, 28
Lu 9:18, 19

f Mt 14:3, 10

g Lu 23:8

h Mk 6:30

i Mt 14:13

j Mt 14:14
Mk 6:34
Yoh 6:2

k Mt 14:15-21
Mk 6:35-44
Yoh 6:5-13

Safu ya 2

a 2Fa 4:42-44

b Mt 14:20
Mk 6:43
Yoh 6:13

c Mt 16:13-16
Mk 8:27-30

d Lu 9:7, 8

e Mt 16:16
Mk 8:29
Yoh 1:41
Yoh 6:68, 69

f Mt 16:20

g Isa 53:5, 8
Lu 17:25

h Mt 16:21
Mk 8:31

i Flp 3:7, 8

akawaambia: “Ninyi wapeni chakula.”^a Wakasema: “Tuna mikate mitano tu na samaki wawili, labda twende tukawanunulie watu hawa wote chakula.” **14** Kwa kweli, kulikuwa na karibu wanaume 5,000. Lakini akawaambia wanafunzi wake: “Waambieni wake ti katika vikundi vya watu hamsini hivosi.” **15** Wakafanya hivyo, na kila mtu akaketi. **16** Akachukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni na kuvibariki. Kisha akavimega, akaanza kuwapa wanafunzi ili wawape watu. **17** Basi wote wakala wakashiba, nao wakakusanya chakula kilichobaki na kujaza vikapu 12.^b

18 Baadaye, alipokuwa akisali akiwa peke yake, wanafunzi wakaja, naye akawaauliza: “Umati unasema mimi ni nani?”^c **19** Wakamjibu: “Yohana Mbatizaji, lakini wengine wanasema Eliya, na bado wengine husema mmoja wa manabii wa kale amefufuliwa.”^d **20** Ndipo akawaauliza: “Hata hivyo, ninyi mnasema mimi ni nani?” Petro akajibu: “Kristo wa Mungu.”^e **21** Ndipo akawaagiza kwa uthabiti wasimwambie mtu yeyote jambo hilo,^f **22** lakini akasema: “Lazima Mwana wa binadamu apatwe na mateso mengi, akataliwe na wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi, kisha atauawa,^g na siku ya tatu atafufuliwa.”^h

23 Ndipo akawaambia wote: “Mtu yeyote akitaka kuni-fuata, lazima ajikane mwenyewe,ⁱ aubebe mti* wake wa mateso siku baada ya

9:23 * Angalia Kamusi, uku. 2012.

siku na aendeleo kunifuata.^a **24** Kwa maana yeyote anayetaka kuuokoa uhai wake* ataupoteza, lakini yeyote anayeupoteza uhai wake* kwa ajili yangu ndiye atakayeuokoa.^b **25** Kwa kweli, mtu atapata faida gani akiupata ulimwengu wote lakini apoteze uhai wake au apate hasara?^c **26** Kwa maana yeyote atakayenionea aibu mimi na maneno yangu, Mwana wa binadamu atamwonea aibu mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wake, na wa Baba, na wa malaika watakatifu.^d **27** Lakini kwa kweli ninawaambia, kuna baadhi ya wale watalosimama hapa ambao hawataonja kifo kamwe kabla ya kuuona Ufalme wa Mungu.”^e

28 Kwa hakika, karibu siku nane baada ya Yesu kusema maneno hayo, alienda mlimani na Petro, Yohana, na Yakobo ili kusali.^f **29** Alipokuwa akisali uso wake ukabadilika, mavazi yake yakawa meupe na kuanza kumetameta. **30** Na tazama! wanaume wawili walikuwa wakizungumza naye; walikuwa Musa na Eliya. **31** Walitokea wakiwa na utukufu na wakaanza kuongea kuhusu kuondoka kwake, ambako kungetimizwa huko Yerusalemu.^g **32** Petro na wenzake walikuwa wamelemewa na usingizi, lakini walipoamka kabisa waliuona utukufu wa Yesu^h na wanau-me wawili waliokuwa wamesimama pamoja naye. **33** Wale wanaume wawili walipokuwa wakiondoka, Petro akamwambia Yesu: “Mwalimu, ni vizuri sisi tuwe hapa. Basi, tu-

9:24 *Au “nafsi yake.”

SURA YA 9

a Mt 10:38
Mt 16:24
Mk 8:34
Lu 14:27

b Mt 16:25
Mk 8:35
Yoh 12:25
Mdo 20:24
Ufu 2:10

c Mt 16:26
Mk 8:36

d Mt 10:33
Mk 8:38
2Ti 2:12

e Mt 16:28
Mk 9:1

f Mt 17:1-8
Mk 9:2-8

g Lu 9:22
Lu 13:33

h 2Pe 1:16

Safu ya 2

a Lu 3:22
Yoh 12:28

b Zb 2:7
Isa 42:1
Mt 3:17
2Pe 1:17

c Kum 18:15
Mt 17:5
Mk 9:7
Mdo 3:22, 23

d Mt 17:9
Mk 9:9

e Mk 9:14, 15

f Mt 17:14-16
Mk 9:17, 18

g Kum 32:5

h Mt 17:17, 18
Mk 9:19-27

tasimamisha mahema mata-tu, moja lako, moja la Musa, na moja la Eliya.” Hakujuu alichokuwa akisema. **34** Lakini alipokuwa akisema mambo haya, wingu likatokea na kuanza kuwafunika. Walipokuwa wakifunikwa na wingu, wakaogopa. **35** Kisha sauti^a ikasikika katika lile wingu iki-sema: “Huyu ni Mwanungu aliyechaguliwa.^b Msikilizeni.”^c **36** Walipokuwa wakisikia ile sauti, wakamwona Yesu akiwa peke yake. Lakini wakakaa kima na katika siku hizo hawakumwambia mtu yeyote lolote kati ya mambo waliyoona.^d

37 Siku iliyofuata, waliposhuka kutoka mlimani, Yesu alikutana na umati mkubwa.^e **38** Na tazama! mtu fulani katika umati akasema kwa sauti kubwa: “Mwalimu, ninakuomba umwangelie mwanangu, kwa sababu yeye ni mwanangu wa pekee.^f **39** Tazama! roho mwovu humshika, naye hupiga kelele ghafla, na humfanya agaegae na kuto-kwa na povu mdomoni, naye hamtoki upesi mpaka anapomjeruhi. **40** Niliwaomba wanafunzi wako wamfukuze, lakini wakashindwa.” **41** Yesu akajibu: “Enyi kizazi kisi-cho na imani na kilichopotoka,^g nitaendelea kuwa pamoja nanyi na kuwavumilia mpaka lini? Mlete mwanao hapa.”^h **42** Lakini alipokuwa akikaribia, yule roho mwovu akamwangusha na kumfanya agaegae sana. Hata hivyo, Yesu akamkemea yule roho mwovu na kumponya mvulana huyo, kisha akamkabidhi kwa baba yake. **43** Wote wakashangazwa na ukuu wa nguvu za Mungu.

Walipokuwa bado wanashangaa kuhusu mambo yote aliyokuwa akifanya, akawaambia wanafunzi wake: **44** "Sikilizeni kwa makini na mkumbuke maneno haya, kwa maana Mwana wa binadamu atasaliwa mikononi mwa watu."^a **45** Lakini hawakuelewa maneno hayo. Kwa kweli, yalifichwa ili wasiyafahamu, nao walio-gopa kumuuliza kuhusu maneno hayo.

46 Kisha wanafunzi wakaanza kubishana kuhusu aliyekuwa mkuu zaidi kati yao.^b

47 Yesu, akijua mawazo ya mioyo yao, akachukua mtoto na kumsimamisha kando yake, **48** akawaambia: "Yeyote anayempokea mtoto huyu kwa msingi wa jina langu ananipokea mimi pia, na yeyote anayenipokea, anampokea pia Yule aliyenituma.^c Kwa maana anayejendesha kama mdogo zaidi kati yenu nyote ndiye mkuu."^d

49 Yohana akasema: "Mwalimu, tulimwona mtu fulani akifukuza roho waovu kwa kutumia jina lako, tukajaribu kumzuia, kwa sababu hafuatani nasi."^e **50** Lakini Yesu akamwambia: "Msijaribu kumzuia, kwa maana yeyote asiyewapinga yuko upande wenu."

51 Wakati ulipokuwa ukikaribia* wa Yesu kwenda mbinguni,^f akaazimia kwenda Yerusalemu. **52** Basi akawatumia wajumbe wamtangulie. Wakaenda katika kijiji kimoja cha Wasamaria, ili wafanye matayarisho kwa ajili yake. **53** Lakini hawakumpokea,^g kwa sababu aliku-

9:51 *Tnn., "ulipotimia."

SURA YA 9

a Mt 17:22, 23
Mk 9:31, 32
Lu 18:31-33

b Mt 18:1-5
Mk 9:33-37
Lu 22:24

c Mk 9:37
Yoh 12:44

d Mt 18:12
Mt 18:4, 5
Mt 23:11, 12

e Mk 9:38-40

f Mdo 1:1, 2
1Ti 3:16

g Yoh 4:9

Safu ya 2

a Mk 3:17

b 2Fa 1:10

c Mt 8:20

d Mt 8:21

e Efe 2:1

f Mt 8:22

g Mwa 19:17

h Mt 10:37
1Ko 9:24
Flp 3:13

SURA YA 10

i Mk 6:7

wa amezimia* kwenda Yerusalemu. **54** Wanafunzi Yakobo na Yohana^a walipoona hilo wakauliza: "Bwana unataka tuagize moto utoke mbinguni uwaangamize?"^b **55** Lakini Yesu akageuka akawakamea. **56** Basi wakaenda kwenye kijiji kingine.

57 Wakiwa njiani, mtu fulani akamwambia Yesu: "Nitakufuata popote utakapoenda."

58 Lakini Yesu akamwambia: "Mbweha wana mapango na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa binadamu hana mahali pa kulaza kichwa chake."^c **59** Kisha akamwambia mtu mwingine: "Njoo, uwe mfuasi wangu." Mtu huyo akasema: "Bwana, niruhusu kwanza niende nikamzike baba yangu."^d **60** Yesu akamwambia: "Waache wafu^e wawazike wafu wao, lakini wewe nenda ukatangaze Ufalme wa Mungu kila mahali."^f **61** Mtu mwingine akamwambia: "Bwana nitakufuata, lakini niruhusu kwanza nika- waage wafu wa nyumbani kwangu." **62** Yesu akamwambia: "Yeyote anayeshika jembe la ng'ombe na kutazama vitu vilivyo nyuma^g hastahili Ufalme wa Mungu."^h

10 Baada ya mambo hayo Bwana akachagua wengine 70, akawatumia wawili wamtangulie katika kila jiji na kila mahali ambako yeye mwenyewe angeenda. **2** Kisha akawaambia: "Ndiyo, mavuno ni mengi, lakini wafanyakazi ni wachache. Kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno awatume

9:53 *Tnn., "alikuwa ameelekeza uso wake."

wafanyakazi katika mavuno yake.^a **3** Nendeni! Tazama! Ninawatuma kama wanakondoo katikati ya mbwamwitu.^b **4** Msibebe mkoba wa pesa wala wafuko wa chakula wala viatu,^c na msimsalimu* mtu yeyote njiani. **5** Mkiingia katika nyumba yoyote, kwanza semeni: 'Nyumba hii na iwe na amani.'^d **6** Na kama humo kuna rafiki wa amani, amani yenu itakaa naye. Lakini kiwa hakuna, itawarudia. **7** Basi kaeni katika nyumba hiyo,^e na mle na kunywa watakachowaandalia,^f kwa maana mfanyakazi anastahili mshahara wake.^g Msihame kutoka nyumba mpaka nyumba.

8 "Pia, mkiingia katika jiji nanyi mkaribishwe, kuleni watakachowapa, **9** na mponye wagonjwa walio huko na kuwaambia: 'Ufalme wa Mungu umekuja karibu nanyi.'^h **10** Lakini mkiingia katika jiji nao wasiwakaribishe, nendeni kwenye barabara zake kuu na kusema: **11** 'Hata mavumbi ya jiji lenu yaliyo kwenye miguu yetu tunayafuta dhidi yenu.ⁱ Hata hivyo jueni kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia.' **12** Ninawaambia kwamba katika siku hiyo, itakuwa afadhali zaidi kwa Sodomu kuliko kwa jiji hilo.^j

13 "Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! kwa sababu kama matendo yenye nguvu yaliyofanywa kwenu yangefanywa huko Tiro na Sidoni, wangekuwa wametubu zamani, wakiwa wamevaa nguo za magunia na kuketi kwenye majivu.^k **14** Kwa hiyo, wakati wa

10:4 *Au "kumsalimu kwa kumkumbatia"

SURA YA 10

- a Mt 9:37, 38
1Ko 3:9
2Th 3:1
- b Mt 10:16
- c Mt 10:9, 10
Lu 9:3
- d Mt 10:12, 13
- e Mt 10:11
Lu 9:4
- f Gal 6:6
- g Mt 10:9, 10
1Ko 9:11, 14
1Ti 5:18
- h Mt 3:1, 2
Lu 9:2
- i Mt 10:14
Lu 9:5
Mdo 13:50, 51
- j Mt 11:24
- k Mt 11:21-23

Safu ya 2

- a Mt 10:40
Mk 9:37
Yoh 13:20
- b Yoh 5:23
Yoh 12:48
Yoh 15:23
- c Mdo 16:17, 18
- d Yoh 12:31
Yoh 16:11
Ebr 2:14
Ufu 12:7-9
- e Zb 91:13
- f Kut 32:32
Da 12:1
Flp 4:3
Ufu 3:5
- g 1Ko 1:19
1Ko 2:6
- h Mt 11:25, 26
- i Yoh 10:15

hukumu itakuwa afadhali zaidi kwa Tiro na Sidoni kuliko kwenu. **15** Nawe Kapernaumu, je, utainuliwa mpaka mbinguni? Utashuka mpaka Kaburini!*

16 "Yeyote anayewasiliza ninyi ananisikiliza mimi pia.^a Na yeyote anayewapuuza ninyi ananipuuza mimi pia. Isitoshe, yeyote anayenipuuza mimi anampuuza pia Yule aliyenituma."^b

17 Ndipo wale 70 wakarudi wakiwa na shangwe, wakisema: "Bwana, hata tunawatiisha roho waovu kwa kutumia jina lako."^c **18** Ndipo akawaambia: "Ninamwona Shetani akiwa tayari ameanzuka^d kutoka mbinguni kama radi. **19** Tazama! Nimewapa mamlaka ya kukanyaga nyoka na nge, na juu ya nguvu zote za adui,^e na hakuna kitu chochote kitakachowadhuru. **20** Hata hivyo, msishangilie kwa sababu mna-watiisha roho waovu, bali shangilien kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni."^f **21** Saa ileile akawa na shangwe kubwa kupitia roho takatifu na kusema: "Ninaku-sifu hadharani, Baba, Bwana wa mbingu na dunia, kwa sababu umewaficha kwa uangalifu mambo haya wenye hekima na wenye akili^g nawe umeyafunua kwa watoto wadogo. Ndiyo, Ee Baba, kwa sababu umekubali iwe hivyo.^h **22** Baba yangu amenikabidhi vitu vyote, na hakuna mtu anayemjua Mwana isipokuwa Baba, wala hakuna anayemjua Baba isipokuwa Mwana,ⁱ na

10:15 *Au "Hadesi." Angalia Kamusi, uku. 2012.

yeyote ambaye Mwana anapenda kumfunulia.”^a

23 Ndipo akawageukia wanafunzi wake faraghani na kuwaambia: “Yenye furaha ni macho yanayoona mambo mnayoona.^b **24** Kwa maana ninawaambia, manabii na wafalme wengi walitamani kuona mambo mnayoona lakini hawakuyaona,^c na kusikia mambo mnayosikia lakini hawakuyasikia.”

25 Tazama! mtu fulani mwenye ujuzi wa Sheria akasimama ili amjaribu, akamuuliza: “Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?”^d

26 Yesu akamuuliza: “Ni mambo gani yameandikwa katika Sheria? Wewe unasomaje?” **27** Akajibu: “Lazima umpedele Yehova* Mungu wako kwa moyo wako wote kwa nafsi[#] yako yote kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote^e na ‘umpedele jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.’”^f **28** Akamwambia: “Umejibu vizuri; endelea kufanya hivyo nawe utapata uzima.”^g

29 Lakini, akitaka kujionyesha kuwa mwadilifu,^h mtu huyo akamuuliza Yesu: “Kwa kweli jirani yangu ni nani?” **30** Yesu akamjibu: “Mtu fulani alikuwa akishuka kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko akavamiwa na wezi, wakamvua nguo, wakampiga, kisha wakamwacha akiwa karibu kufa. **31** Ikatukia kwamba kuhani fulani alikuwa akishuka katika barabara hiyo, lakini alipomwona yule mtu akapi-

10:27 *Angalia Nyongeza A5. [#]Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 10

a Mt 11:27
Yoh 1:18
2Ko 4:6

b Mt 13:16,17

c 1Pe 1:10,11

d Mt 19:16
Mk 10:17
Lu 18:18

e Kum 6:5
Kum 10:12
Yos 22:5
Mk 12:30

f Law 19:18
Mt 19:19
Ro 13:9
Gal 5:14
Yak 2:8

g Law 18:5
Yoh 17:3

h Lu 16:15

Safu ya 2

a Yoh 4:9

b Mt 19:19

c Met 14:21

d Lu 6:36
Yoh 13:17
Efe 4:32

e Yoh 12:2

ta upande mwingine wa barabara. **32** Vivyo hivyo, Mlawi alipofika mahali hapo na kumwona, akapita upande mwingine wa barabara. **33** Lakini Msamaria^a fulani aliyekuwa akisafiri kwenye barabara hiyo alipomwona, akamsikitikia. **34** Basi akamkaribia akayamwagia majeraha yake mafuta na divai, kisha akayafunga. Akampandisha kwenye punda wake akampeleka kwenye nyumba ya wageni na kumtunza. **35** Siku iliyofuata akamlipa msimamizi wa nyumba hiyo dinari* mbili, akamwambia: ‘Mtunze, nami nita-kulipa gharama zozote za ziada nitakaporudi.’ **36** Kati ya watu hao watatu, unafikiri ni nani aliyekuwa jirani^b ya mtu aliyevamiwa na wezi?” **37** Akajibu: “Ni yule aliyemtendea kwa rehema.”^c Ndipo Yesu akamwambia: “Nenda ukafanye vivyo hivyo.”^d

38 Walipoendelea na safari, wakaingia katika kijiji fulani. Mwanamke aliyelitwa Martha^e akamkaribisha Yesu nyumbani kwake. **39** Martha alikuwa na dada aliyelitwa Maria, ambaye aliketika miguuni pa Bwana akisikiliza alichokuwa akisema.* **40** Lakini Martha alikengeushwa na kazi nyingi. Basi, akaja na kusema: “Bwana, hujali kwamba dada yangu ameniacha nishughulike peke yangu? Mwambie aje anisaidie.” **41** Bwana akamjibu: “Martha, Martha, unasumbuka na kuhangaikia mambo mengi. **42** Ni vitu vichache tu vinavyohitajiwa au kimoja

10:35 *Angalia Nyongeza B14. 10:39 *Tnn., “neni lake.”

tu. Maria alichagua fungu zuri,*^a nalo halitaondolewa kwake.”

11 Sasa alikuwa mahali fulani akisali, alipomaliza, mmoja wa wanafunzi wake akamwambia: “Bwana, tufundishe jinsi ya kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake.”

2 Basi akawaambia: “Mnaposali, semeni, ‘Baba, jina lako na litakaswe.*^b Ufalme wako na uje.^c **3** Kila siku utupatie mkate wetu kulingana na mahitaji yetu.^d **4** Na utusamehe dhambi zetu,^e kwa maana sisi pia humsamehe kila mtu aliye na deni letu;^f na usituingize katika majaribu.”^g

5 Kisha akawaambia: “Ikiwa mmoja wenu ana rafiki, naye aende kwake katikati ya usiku na kumwambia, ‘Rafiki, niko peshe mikate mitatu, **6** kwa sababu rafiki yangu amekuja kwangu kutoka safarini nami sina kitu cha kumpa.’ **7** Lakini yule aliye ndani amjibu: ‘Acha kunisumbua. Tayari mlango umefungwa, nami na watoto wangu tumelala. Siwezi kuamka nikupe chocho.’ **8** Ninawaambia ingawa hataamka na kumpa chocho kwa sababu yeye ni rafiki yake, kwa hakika ataamka na kumpa kwa sababu anaendelea^h kumwomba. **9** Basi ninawaambia, endeleeni kuomba,ⁱ nanyi mtapewa; endeleeni kutafuta, nanyi mtapata; endeleeni kupiga hodi, nanyi mtafunguliwa.^j **10** Kwa maana kila mtu anayeomba hupokea,^k na kila mtu anayeta-

10:42 *Au “fungu bora.” 11:2 *Au “litukuzwe; lionwe kuwa takatifu.”

SURA YA 10

a Mt 4:4
Mt 6:33

SURA YA 11

b Law 22:32
Isa 5:16
Eze 36:23

c Da 2:44
Da 7:13, 14
Mt 6:9-13

d Zb 37:25

e Zb 79:9
Da 9:19

f Mk 11:25
Efe 4:32
Kol 3:13

g Lu 22:46
1Ko 10:13
Yak 1:13
Ufu 3:10

h Lu 18:5

i Ro 12:12

j Mt 7:7, 8

k Mk 11:24
Yoh 15:7
Yak 1:6
1Yo 3:22
1Yo 5:14

Safu ya 2

a Mt 7:9, 10

b Mt 7:11
Yak 1:17

c Mt 12:22

d Mt 9:32-34

e Mt 12:24-30
Mk 3:22-27

f Mt 12:38
Mk 8:11

g Yoh 2:24, 25

h Kut 8:19

i Mt 12:28
Lu 17:21

futa hupata, na kila mtu anayepiga hodi atafunguliwa. **11** Kwa kweli, ni baba gani kati yenu ambaye mwana wake akiomba samaki, atampa nyoka?^a **12** Au pia akiomba yai, atampa nge? **13** Kwa hiyo, ingawa ninyi ni waovu, mnajua jinsi ya kuwapa watoto wenu zawadi nzuri, je, Baba aliye mbinguni hatawapa hata zaidi roho takatifu wale wanaomwomba!”^b

14 Baadaye alimfukuza roho mwovu aliye bubu.^c Roho huyo mwovu alipotoka, yule bubu akazungumza. Nao umati ukashangaa.^d **15** Lakini baadhi yao wakasema: “Anawafukuza roho wenu kwa nguvu za Beelzebuli,* mtawala wa roho waovu.”^e **16** Na wengine, ili kumjaribu, wakamwomba afaanye ishara^f kutoka mbinguni. **17** Akijua mawazo yao,^g akawaambia: “Kila ufalme ulioga-wanyika dhidi yake wenyewe utaangamia, na nyumba iliyo-gawanyika dhidi yake yenyewe itaanguka. **18** Vivyo hivyo, ikiwa Shetani amegawanyika dhidi yake mwenyewe, ufalme wake utawezaje kusimama? Kwa maana mnasema ninafukuza roho waovu kupitia Beelzebuli. **19** Ikiwa ninawafukuza roho waovu kupitia Beelzebuli, wana wenu wanawafukuza kupitia nani? Hiyo ndiyo sababu watakuwa wamuzi wenu. **20** Lakini ikiwa ninawafukuza roho waovu kupitia kidole cha Mungu,^h kwa kweli Ufalme wa Mungu umewafikia ninyi ghafla.ⁱ **21** Mtu mwenye nguvu aliye na silaha, anapolinda jumba lake, mali yake huwa salama. **22** Laki-

11:15 *Jina lingine la Shetani.

ni mtu mwingine mwenye nguvu zaidi yake anapomshambulia na kumshinda, humnya-ng'anya silaha zake zote alizotegemea, naye hugawa vitu alivyompora. **23** Yeyote asiye upande wangu ananipinga, na yeyote asiyekusanya pamoja nami anatawanya.^a

24 "Roho mwovu anapotoka mtu, yeye hupitia mae-neo yasiyo na maji akitafuta mahali pa kupumzika, lakini anapokosa yeye husema, 'Nitarudi kwenye nyumba yangu niliyoihama.'^b **25** Anapofika hukuta nyumba ikiwa imefagiwa ikawa safi na kupambwa. **26** Kisha huenda na kuwaleta roho wengine saba walio waovu kuliko yeye, na baada ya kuingia ndani, wao hukaa humo. Basi hali ya mwisho ya mtu huyo huwa mbaya zaidi kuliko ya kwanza."

27 Alipokuwa akisema mambo hayo mwanamke fulani katika umati akasema kwa sauti kubwa: "Lenye furaha ni tumbo lililokubeba wewe na matiti uliyonyonya!"^c **28** Lakini Yesu akasema: "Hapana, badala yake, wenye furaha ni wale wanaolisikia neno la Mungu na kulishika!"^d

29 Umati ulipozidi kuongezeka, akaanza kusema: "Kizazi hiki ni kiovu; kinatafuta ishara, lakini hakitapewa ishara yoyote isipokuwa ishara ya Yona.^e **30** Kwa maana kama vile Yona^f alivyokuwa ishara kwa Waninawi, ndivyo Mwana wa binadamu atakavyokuwa kwa kizazi hiki. **31** Malkia wa kusini^g atasimamishwa katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki naye atakihukumu kwa saba-

SURA YA 11

a Mt 12:30

b Mt 12:43-45

c Lu 1:46-48

d Kum 29:9

Zb 1:1, 2

Zb 112:1

Zb 119:2

Mt 7:21

Yak 1:25

e Mt 12:38-42

Mt 16:4

f Yon 1:17

g 1Fa 10:1

2Nya 9:1

Safu ya 2

a Mt 12:42

b Yon 3:5

c Mt 5:15

Mk 4:21

Lu 8:16

d Mt 6:22, 23

e Mt 15:2

f Mt 23:25, 26

bu alikuja kutoka miisho ya dunia ili asikie hekima ya Sulemani. Lakini tazama! hapa pana mtu mkuu kuliko Sulemani.^a **32** Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki nao watakihukumu, kwa sababu walitubu Yona alipowahubiria.^b Lakini tazama! hapa pana mtu mkuu kuliko Yona. **33** Hakuna mtu anayewasha taa na kui-ficha au kuiweka chini ya kikapu,* bali huiweka kwenye kinara cha taa,^c ili iwaangazie wale wanaoingia. **34** Taa ya mwili ni jicho lako. Ikiwa jicho lako linakazia jambo hususa,* mwili wako wote utakuwa mwangavu,^d lakini ikiwa lina wivu,^e mwili wako utakuwa na giza.^d **35** Basi, uwe mwangalifu ili nuru iliyo ndani yako isiwe ni giza. **36** Kwa hiyo, ikiwa mwili wako wote ni mwangavu bila giza lolote, utakuwa mwangavu kama taa inapokuangazia kwa mwanga wake."

37 Baada ya kusema hayo, Farisayo mmoja alimwomba ale pamoja naye. Basi Yesu akaingia na kuketi meza ni. **38** Hata hivyo, Farisayo huyo akashangaa kuona kwamba Yesu hakunawa* kabla ya kula.^e **39** Lakini Bwana akamwambia: "Ninyi Mafarisayo, husafisha upande wa nje wa kikombe na sahani, lakini ndani yenu mmejaa pupa na uovu.^f **40** Enyi wapumbavu! Yule aliyetengeneza nje ndiye aliyetengeneza ndani pia, sivyo? **41** Lakini toeni vitu

11:33 *Au "kikapu cha kupimia." **11:34**

*Au "linaona vizuri." Tnn., "ni rahisi." *Au "utajawa na nuru." [^]Tnn., "ni baya; lina uovu." **11:38** *Yaani, hakuji-safisha kisherehe.

vilivyo ndani viwe zawadi za rehema,* na tazama! mtakuwa safi katika mambo mengine yote. **42** Lakini ole wenu Mafarisayo, kwa sababu mnatoa sehemu ya kumi ya mnanaa na mchicha na kila aina ya mbo-ga,^a lakini mnapuuza haki na kumpenda Mungu! Mlipaswa kufanya mambo hayo, bila kupuuza yale mengine.^b **43** Ole wenu Mafarisayo, kwa sababu mnapenda viti vya mbele* katika masinagogi na kusalimiwa sokoni!^c **44** Ole wenu, kwa sababu ninyi ni kama makaburi* yasiyoonekana,^{#d} ambayo watu hutembea juu yake bila kujua!”

45 Mtu fulani mwenye ujuzi wa Sheria akanwambia: “Mwalimu, unaposema mambo hayo, unatutukana sisi pia.”

46 Ndipo akasema: “Ole wenu pia ninyi mlio na ujuzi wa Sheria, kwa sababu mnawatwika watu mizigo mizito, lakini ninyi wenyewe hamwigusi hata kwa kidole kimoja!^e

47 “Ole wenu, kwa sababu mnajenga makaburi* ya manabii ambao mababu zenu waliwaua!^f **48** Hakika ninyi ni mashahidi wa matendo ya mababu zenu nanyi mnakubaliana nao, kwa sababu waliwaua manabii^g nanyi mna-jenga makaburi yao. **49** Kwa sababu hiyo hekima ya Mungu ilisema: ‘Nitawatuma manabii na mitume kwao, lakini watawaua na kuwatesa baadhi yao, **50** ili damu ya manabii wote iliyomwagwa tangu

11:41 *Au “ili kuwapa maskini zawadi.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 11:43 *Au “vilivyo bora.” 11:44, 47 *Au “makaburi ya ukumbusho.” 11:44 #Au “makaburi yasiyo na alama.”

SURA YA 11

a Law 27:30

b Mt 23:23, 24
Yoh 7:24

c Mt 23:6, 7

d Mt 23:27, 28

e Mt 23:2, 4

f Mt 23:29-31

g Mdo 7:52
Ebr 11:32, 37

Safu ya 2

a Ufu 18:21, 24

b Mwa 4:8, 10

c 2Nya 24:20-22

d Mt 23:13
1Th 2:14-16

e Lu 20:20

SURA YA 12

f Mt 16:6
Mk 8:15

g Mt 10:26, 27
Mk 4:22
Lu 8:17

h Yoh 15:14

i Mdo 20:24

j Mt 10:28

kuwekwa msingi wa ulimwengu idaiwe kutoka kwa kizazi hiki,^a **51** kuanzia damu ya Abeli^b mpaka damu ya Zekaria, aliyeuawa kati ya madhabu na ile nyumba.’*^c Ndiyo, ninawaambia, kizazi hiki kitadaiwa[#] damu hiyo.

52 “Ole wenu ninyi wenye ujuzi wa Sheria, kwa sababu mliuondoa ufunguo wa ujuzi. Ninyi hamkuingia, na mnawa-zuia wale wanaoingia!”^d

53 Basi alipotoka hapo, waandishi na Mafarisayo wakaa-nda kumsonga sana na kumuuliza maswali mengi, **54** waki-mtega ili wamnase kwa mane-no yake.^e

12 Wakati huo, maelfu ya watu walikusanyika hata wakawa wanakanyaga-na, Yesu akaanza kuzungu-mza kwanza na wanafunzi wake: “Jihadharini na cha-chu ya Mafarisayo, ambayo ni unafiki.^f **2** Lakini haku-na jambo lolote lililofunikwa kwa uangalifu ambalo halita-funuliwa, na hakuna siri yo-yote ambayo haitafichuliwa.^g

3 Kwa hiyo, mambo mnayo-sema gizani yatasikiwa nuru-ni, na mambo mnayonong’o-na katika vyumba vya fara-gha yatahubiriwa juu ya paa za nyumba. **4** Isitoshe, nina-waambia ninyi, rafiki zangu,^h msiwaogope wale wanaoua mwili na baada ya hilo hawa-wezi kufanya jambo lolote zai-di.ⁱ **5** Lakini nitawaonyesha yule mwanepaswa kumwogo-pa: Mwagopeni yule ambaye baada ya kuua ana mamlaka ya kutupa ndani ya Gehena.*^j

11:51 *Au “hekalu.” #Au “kitashtaki-wa.” 12:5 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

Ndiyo, ninawaambia, mwogopeni Huyo.^a **6** Shore watano huuzwa kwa sarafu mbili za thamani ndogo,* sivyo? Na bado Mungu hamsahau[#] hata mmoja.^b **7** Lakini hata nywele zote za vichwa vyenu zimehesabiwa.^c Msiogope; ninyi ni wenye thamani kuliko shore wengi.^d

8 "Ninawaambia, kila mtu anayenikiri mbele ya watu,^e Mwana wa binadamu pia atamkiri mbele ya malaika wa Mungu.^f **9** Lakini yeyote anayenikana mbele ya watu atakana mbele ya malaika wa Mungu.^g **10** Na kila mtu anayesema neno baya kumhusu Mwana wa binadamu atasamehewa, lakini yeyote anayeikufuru roho takatifu hatasamehewa.^h **11** Mtakapopelekwa mbele ya makusanyiko ya watu wote,* maofisa wa serikali, na mamlaka, msihangaike kuhusu jinsi mtakavyojitetea au jambo mtakalosema,ⁱ **12** kwa maa-na saa hiyohiyo roho takatifu itawafundisha mambo mnayopaswa kusema."^j

13 Kisha mtu fulani katika umati akawambia: "Mwalimu, mwambie ndugu yangu tugawane urithi." **14** Akawambia: "Ni nani aliyeniweka niwe mwamuzi au mpatanishi kati yenu wawili?" **15** Ndipo akawaambia: "Endeleeni kufungua macho yenu na mjilinde na kila aina ya pupa,*^k kwa sababu hata mtu anapokuwa na vitu vingi, uhai wake hautokani na vitu alivyo navyo."^l **16** Ndipo akawaambia mfano

12:6 *Tnn., "kwa sarafu mbili za asarioni." Angalia Nyongeza B14. ^aAu "hampuuzi." 12:11 *Au labda "masinagogli." 12:15 *Au "tamaa."

SURA YA 12

a Isa 8:13
Ebr 10:31
1Pe 2:17
Ufu 14:7

b Mt 10:29

c Mt 10:30
Lu 21:18

d Mt 10:31
Lu 12:24

e Ro 10:9

f Mt 10:32, 33

g Mk 8:38
Lu 9:26
2Ti 2:12
1Yo 2:23

h Mt 12:31, 32
Mk 3:28, 29

i Mt 10:19, 20
Mk 13:11
Lu 21:14, 15

j Kut 4:12
Mdo 6:8, 10

k Kut 20:17
Kum 5:21
Kol 3:5

l 1Ti 6:7

Safu ya 2

a Yak 4:13-16

b Zb 49:16-19
Met 27:1

c Mhu 11:9
Mt 6:20
1Ti 6:17-19
Yak 2:5

d Mt 6:25-30
Flp 4:6

e Ayu 38:41
Zb 147:9

f Mt 6:26
Lu 12:7

huu: "Shamba la tajiri fulani lilizaa vizuri. **17** Basi akanza kuwaza moyoni, 'Nitafanya nini kwa sababu sina mahali pa kuhifadhi mazao yangu?' **18** Kisha akasema, 'Nitafanya hivi:^a Nitabomoa maghala yangu na kujenga makubwa zaidi, kisha nitahifadhi humo nafaka yangu na vitu vyangu vyote, **19** kisha nitajiambia:* "Una[#] vitu vingi vizuri ulivyokusanya kwa miaka mingi; starehe, ule, unywe, na ujifurahishe.'" **20** Lakini Mungu akawambia, 'Wewe mpu mbavu, usiku huu wanataka uhai wako.* Basi, vitu ulivyohifadhi vitakuwa vya nani?'^b **21** Hivyo ndivyo huwa kwa mtu anayejiwekea hazina lakini si tajiri kwa Mungu."^c

22 Kisha akawaambia wanafunzi wake: "Ndiyo sababu ninawaambia, acheni kuhangaikia uhai wenu* kuhusu kile mtakachokula au mili yenu kuhusu kile mtakachovaa.^d **23** Kwa maa-na uhai una* thamani kuliko chakula na mwili kuliko mavazi. **24** Waangalieni kunguru: Hawapandi mbegu wala hawavuni; hawana bohari wala ghala; lakini Mungu huwalisha.^e Je, ninyi si wenye thamani kuliko ndege?^f **25** Ni nani kati yenu ambaye kwa kuhangaika anaweza kurefusha uhai wake kwa mkono* mmoja? **26** Basi, kama hamwezi kufanya jambo dogo kama hilo, kwa nini mhangaikie yale mambo

12:19 *Au "nitaiambia nafsi yangu."^a [#]Au "Nafsi, una" 12:20 *Au "nafsi yako." 12:22 *Au "nafsi zenu." 12:23 *Au "nafsi ina." 12:25 *Angalia Nyongeza B14.

mengine?^a **27** Angalieni jinsi mayungiyungi* yanavyokua: Hayafanyi kazi wala hayasokoti; lakini ninawaambia hata Sulemani katika utukufu wake wote hakupambwa kama maua hayo.^b **28** Basi, ikiwa Mungu huivika hivyo mimea ya shambani, ambayo ipo leo na kesho hutupwa ndani ya jiko, je, hatawavika vizuri zaidi ninyi wenye imani ndogo? **29** Basi acheni kutafuta kile mtakachokula au mtakachokunywa, na acheni kuhangaika kwa wasiwasi;^c **30** kwa maana mataifa yanatafuta vitu hivi vyote kwa bidii, lakini Baba yenu anajua mnahitaji vitu hivi.^d **31** Badala yake, endeeleni kuutafuta Ufalme wake, nanyi mtaongezewa vitu hivyo.^e

32 "Msiogope, ninyi kundi dogo,^f kwa sababu Baba yenu amekubali kuwapa Ufalme.^g **33** Uzeni mali zenu na kutoa zawadi za rehema.^{*h} Tengenezeni mikoba ya pesa isiyochakaa, hazina isiyopungua huko mbinguni,ⁱ ambako mwizi hawezi kufika wala nondo[#] hali. **34** Kwa maana mahali ilipo hazina yenu, ndipo mioyoyenu itakapokuwa.

35 "Vaeni mavazi, muwe tayari^{*j} na mwashe taa zenu,^k **36** nanyi muwe kama watu wanaomsubiri bwana wao arudi^l kutoka kwenye karamu ya ndoa,^m ili atakapokuja na kupiga hodi wamfungulie mara moja. **37** Wenye furaha ni watumwa ambao bwa-

12:27 *Aina ya maua. 12:33 *Au "kuwapa maskini zawadi." Angalia Kamusi, uku. 2012. #Aina ya wadudu. 12:35 *Tnn., "Jifungeni mishipi viunoni."

SURA YA 12

- a Mt 6:34
- b 1Fa 10:4-7
- c Mt 6:31, 32
- d 2Nya 16:9
Flp 4:19
- e Zb 34:10
Mt 6:33
1Ti 4:8
- f Yoh 10:14
- g Da 7:27
Lu 22:28-30
Ebr 12:28
Yak 2:5
Ufu 1:6
- h Mt 19:21
Lu 18:22
Mdo 2:45
Mdo 4:34, 35
- i Mt 6:20, 21
Lu 16:9
1Ti 6:18, 19
- j Efe 6:14
1Pe 1:13
- k Mt 25:1
Flp 2:15
- l Mk 13:35
- m Mt 25:5

Safu ya 2

- a Mt 24:43
1Th 5:2
2Pe 3:10
Ufu 16:15
- b Mt 24:44
Mt 25:13
Ufu 3:3
- c Mt 24:45-47
- d Mt 24:48-51

na wao akija atawakuta wakikesha! Kwa kweli ninawaambia, atavaa vazi la mhudumu* na kuwaambia waketi mezani naye atakuja na kuwahudumia. **38** Akija katika kesha la pili,^{*} au hata kesha la tatu,[#] na kuwakuta wakiwa tayari, watakuwa wenye furaha! **39** Lakini jueni jambo hili, ikiwa mwenye nyumba angejua saa ambayo mwizi angekuja, hangeruhusu nyumba yake ivunjwe.^a **40** Ninyi pia, endeeleni kuwa tayari, kwa sababu Mwana wa binadamu atakuja saa msiyotazamia.^b

41 Ndipo Petro akamuuliza: "Bwana, unatuambia sisi tu mfano huo au watu wote pia?" **42** Bwana akasema: "Kwa kweli ni nani msimamizi* mwaminifu, mwenye busara,[#] ambaye bwana wake atamweka asimamie watumishi[^] wake na kuendelea kuwapa kipimo chao cha chakula kwa wakati unaofaa?^c **43** Mwenye furaha ni mtumwa huyo, ikiwa bwana wake atakapokuja atamkuta akifanya hivyo! **44** Kwa kweli ninawaambia, atamweka rasmi asimamie mali zake zote. **45** Lakini ikiwa mtumwa huyo atasema moyoni mwake, 'Bwana wangu anakawia kuja,' naye aanze kuwapiga watumishi wa kiume na wa kike na kula na kunywa na kulewa,^d **46** bwana wa mtumwa huyo atakuja siku asiyomtazamia na katika saa asiyojua, naye atamwadhi-

12:37 *Au "atajifunga kiunoni." 12:38 *Kuanzia saa 3 usiku mpaka saa 6 usiku. #Kuanzia saa 6 usiku mpaka saa 9 usiku. 12:42 *Au "msimamizi wa nyumba." #Au "mwenye hekima." ^Au "watumishi wa nyumbani."

bu kwa ukali na kumweka pamoja na wasio waaminifu. **47** Mtumwa huyo aliyeelewa mapenzi ya bwana wake lakini hakujitayarisha wala kufanya alichambiwa* atapigwa sana.^a **48** Lakini yule ambaye hakuelewa na hivyo akafanya mambo yanayostahili adhabu atapigwa kidogo. Kwa kweli, kila mtu ambaye alipewa mengi atadaiwa mengi, na yule aliyewekwa kusimamia mengi, atadaiwa mengi kuliko ilivyo kawaida.^b

49 "Nilikuja kuwasha moto duniani, na kama tayari ume-waka, ninahitaji nini kingine? **50** Kwa kweli, kuna ubatizo ninaopaswa kubatizwa, na ninataabika sana mpaka umalizike!^c **51** Je, mnafikiri nilikuja kuleta amani duniani? Hapana, si amani bali mgawanyiko.^d **52** Kuanzia sasa kutakuwa na watu watano katika nyumba moja waliogawanyika, watatu dhidi ya wawili na wawili dhidi ya watatu. **53** Watagawanyika, baba dhidi ya mwana, mwana dhidi ya baba, mama dhidi ya binti, binti dhidi ya mama, mama mkwe dhidi ya binti mkwe, na binti mkwe dhidi ya mama mkwe."^e

54 Kisha akauambia umati: "Mnapoona wingu likitokea magharibi, mara moja mnasema, 'Kutakuwa na dhoruba,' na inakuwa hivyo. **55** Nanini mnapoona upepo wa kusini ukivuma, ninyi husema, 'Kutakuwa na joto sana,' na inakuwa hivyo. **56** Wanafiki, mnajua jinsi ya kuchunguza dunia na anga, lakini kwa nini hamjui jinsi ya kuchu-

12:47 * Au "kufanya mapenzi yake."

SURA YA 12

a Yak 1:22
Yak 4:17

b Mt 25:29
Yoh 15:2

c Yoh 12:27

d Mt 10:34-36
Yoh 7:41, 43
Yoh 9:16

e Mik 7:6

Safu ya 2

a Mt 16:2, 3
Lu 19:42

b Mt 5:25, 26

SURA YA 13

c Mdo 3:19

d Mt 21:19
Mk 11:13

nguzi kinachotendeka wakati huu?^a **57** Kwa nini hamtambui pia mambo yaliyo ya uadilifu? **58** Kwa mfano, unapoenda kwa mtawala pamoja na mtu anayekushtaki, anza kusuluhisha mambo pamoja naye mkiwa njiani, ili asikupeleke mbele ya hakimu, naye hakimu akukabidhi kwa ofisa wa mahakama, naye ofisa wa mahakama akutupe gerezani.^b **59** Ninakuambia, hakika hutatoka humo mpaka utakapolipa sarafu* yako ndogo ya mwisho."

13 Wakati huo, watu fulani waliokuwa hapo walimwambia Yesu kuhusu Wagalilaya ambao Pilato alikuwa amechanganya damu yao na dhabihu zao. **2** Akawaambia: "Je, mnafikiri Wagalilaya hao walikuwa watenda dhambi wabaya zaidi kuliko Wagalilaya wengine wote kwa sababu walipatwa na mambo hayo? **3** Hapana. Ninawaambia msipotubu, nyote mtaangamizwa vivyo hivyo.^c **4** Au wale 18 walioangukiwa na mnara huko Siloamu wakafa, je, mnafikiri walikuwa na hatia kuliko watu wengine wote wanaoishi Yerusalemu? **5** Hapana, ninawaambia; msipotubu, ninyi pia mtaangamizwa kama wao."

6 Kisha akawaambia mfano huu: "Mtu fulani alikuwa na mtini uliopandwa katika shamba lake la mizabibu, akaenda kutafuta matunda kwenye mti huo lakini hakupata.^d **7** Ndipo akamwambia mtunza-mizabibu, 'Kwa miaka mitatu nimekuwa nikija kutafuta matunda kwenye mtini

12:59 * Tnn., "leptoni ya mwisho." Angalia Nyongeza B14.

huu, lakini sijayapata. Ukate! Kwa nini uendeleo kuharibu ardhi? **8** Akamjibu, 'Bwana, uache kwa mwaka mwingine mmoja niupalilie na kuutia mbolea. **9** Ukizaa matunda wakati uja, vema; la sivyo, utaukata.'^a

10 Sasa Yesu alikuwa akifundisha katika sinagogi siku ya Sabato. **11** Na tazama! hapo palikuwa na mwanamke aliyekuwa na roho ya udhaifu* kwa miaka 18, mwili wake ulikuwa umepindika na hangeweza kusimama wima. **12** Yesu alipomwona, akamwambia: "Mwanamke, umefunguliwa kutoka kwa udhaifu wako."^b **13** Yesu akaweka mikono juu ya yule mwanamke na mara moja akanyooka na kuanza kumtukuza Mungu. **14** Lakini ofisa msimamizi wa sinagogi akakasirika kwa sababu Yesu aliponya siku ya Sabato, akauambia umati: "Kuna siku sita za kufanya kazi;^c basi, njooni mponywe katika siku hizo, bali si siku ya Sabato."^d **15** Hata hivyo, Bwana akajibu: "Wanafiki,^e je, kila mmoja wenu hamfungui ng'ombe au punda wake kutoka kwenye kibanda siku ya Sabato na kumpeleka akanywe maji?" **16** Je, haifai kwa mwanamke huyu, binti ya Abrahamu, ambaye Shetani alikuwa amemfunga kwa miaka 18 afunguliwe kutoka kwenye kifungo hicho siku ya Sabato?" **17** Aliposema mambo hayo, wapinzani wake wakaaanza kuaibika, lakini umati wote ukaanza kushangilia ulipoona mambo yenye utukufu aliyofanya.⁹

13:11 *Au "roho mwovu aliyemlemaza."

SURA YA 13

a 2Pe 3:9

b Isa 61:1
Lu 4:18

c Kut 20:9,10
Kut 35:2
Kum 5:13,14

d Mt 12:10
Mk 3:2
Yoh 5:15,16

e Mt 23:27,28
Lu 12:1

f Lu 14:5

g Lu 9:43

Safu ya 2

a Mt 13:31,32
Mk 4:30-32

b Mt 13:33

c Isa 55:6
Mt 7:13,14
Flp 3:12-14
1Ti 6:12

d Lu 6:46

e Mt 7:22,23

18 Basi akaendelea kusema: "Ufalme wa Mungu unafanana na nini, nitaulinganisha na nini? **19** Ni kama mbe-gu ya haradali ambayo mtu alichukua na kuipanda kati-ka shamba lake, ikasitawi na kuwa mti, nao ndege wa angani wakajenga viota kwenye matawi yake."^a

20 Akauliza tena: "Nitaulinganisha Ufalme wa Mungu na nini? **21** Ni kama chachu* ambayo mwanamke alichukua na kuichanganya na vipimo[#] vitatu vikubwa vya unga mpa-ka unga wote ukachacha."^{△b}

22 Alipokuwa akisafiri kwen-nda Yerusalemu, Yesu alipita kutoka jiji mpaka jiji na kuto-ka kijiji mpaka kijiji akiwafun-disha watu. **23** Sasa mtu fu-lani akamuuliza: "Bwana, je, wale watakaookolewa ni wa-chache?" Yesu akawaambia: **24** "Jitahidini sana ili mwinge kupitia mlango mwemba-mba,^c kwa sababu ninawaa-ambia wengi watajaribu kuingia lakini hawataweza. **25** Mwe-nye nyumba atakaposimama na kuufunga mlango, mtakuwa nje mkibisha mlagoni, mkise-ma, 'Bwana, tufungulie.'^d La-kini atawajibu: 'Sijui mnato-ka wapi.' **26** Kisha mtamjibu, 'Tulikula na kunywa pamoja nawe, nawe ulifundisha katika barabara zetu kuu.'^e **27** Laki-ni atawaambia, 'Sijui mnato-ka wapi. Ondokeni kwangu, ni-nyi nyote watenda maovu!' **28** Hapo ndipo mtalia na ku-saga mena yenu mtakapoona Abrahamu, Isaka, Yakobo, na

13:21 *Au "hamira." [#]Tnn., "vipimo vya sea." Sea moja ilikuwa sawa na kilo-gramu 3.3 au lita 7.33. Angalia Nyonge-za B14. [△]Au "ukaumuka."

manabii wote katika Ufalme wa Mungu, lakini ninyi mkiwa mmetupwa nje.^a **29** Isitoshе, watu watakuja kutoka mashariki na magharibi, na kutoka kaskazini na kusini, nao wataketi mezani katika Ufalme wa Mungu. **30** Tazama! kuna wale wa mwisho watakaokuwa wa kwanza, na kuna wale wa kwanza watakaokuwa wa mwisho.”^b

31 Saa ileile baadhi ya Mafarisayo wakaja na kumwambia: “Ondoka hapa uende mahali pengine, kwa sababu Herode anataka kukuu.” **32** Akawaambia: “Nendeni mkamwambie mbweha huyo, ‘Tazama! Ninawafukuza roho waovu na kuwaponya watu leo na kesho, na siku ya tatu nitakuwa nimemaliza.’ **33** Hata hivyo, lazima niendeleo leo, kesho, na keshokutwa, kwa sababu haiwezekani* nabii kuuawa nje ya Yerusalemu.^c **34** Yerusalemu, Yerusalemu, muuaji wa manabii na aliyewapiga mawe wale waliotumwa kwake^d—nilijariibu mara ngapi kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku anavyokusanya vifaranga wake chini ya mabawa yake! Lakini hamkutaka.^e **35** Tazama! Mmeachiwa nyumba yenu.^f Ninawaambia, hamtationa tena mpaka mtakaposema, ‘Amebarikiwa yule anayekuja katika jina la Yehova!’”^g

14 Siku moja ya Sabato, Yesu alienda kula kaka katika nyumba ya kiongozi mmoja wa Mafarisayo, nao walikuwa wakimtamaza

13:33 *Au “ni jambo lisilowaziwa.”
13:35 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 13

a Mt 8:11, 12

b Mt 19:30
Mk 10:31

c Mt 16:21

d 2Nya 24:20, 21
Ne 9:26

e Mt 23:37

f Law 26:31
1Fa 9:7, 8
Yer 12:7
Yer 22:5g Zb 118:26
Mt 23:38, 39

Safu ya 2

SURA YA 14

a Lu 6:9
Yoh 7:23b Kut 23:5
Kum 22:4c Mt 12:11
Lu 13:15d Mt 23:2, 6
Lu 11:43
Lu 20:46

e Met 25:6, 7

f Met 15:33
Yak 4:10
1Pe 5:5g Met 29:23
Mt 23:12
Lu 18:14
Yak 4:6

sana. **2** Tazama! mbele yake kulikuwa na mtu mwenye ugonjwa wa kuvimba mwili.*

3 Basi Yesu akawauliza wale wenye ujuzi wa Sheria na Mafarisayo: “Je, ni halali au si halali kumponya mtu siku ya Sabato?”^a **4** Lakini wakanyamaza. Basi akamshika mtu huyo, akamponya na kumwambia aende zake. **5** Kisha akawauliza: “Ni nani kati yenu ambaye mwana wake au ng’ombe wake akianguka ndani ya kisima^b siku ya Sabato, hatamtoa humo mara moja?”^c **6** Wakashindwa kumjibu.

7 Kisha akawapa mfano watu walioalikwa, alipona jinsi walivyokuwa wakichagua kuketi mahali pa heshima zaidi.^d Akawaambia: **8** “Mtu akikualika kwenye karamu ya ndoa, usiketi mahali pa heshima zaidi.^e Huenda pia amemwalika mtu mashuhuri kuliko wewe. **9** Naye aliyewaalika atakuja kukuambia, ‘Mwachie mtu huyu mahali ulipoketi.’ Kisha utaondoka kwa aibu na kuketi mahali pa chini kabisa. **10** Lakini unapoalikwa, nenda uketi mahali pa chini kabisa, ili mtu aliyekualika akija akuambie, ‘Rafiki yangu, nenda uketi mahali pa heshima zaidi.’ Kisha utakuwa na heshima mbele ya wageni wenzako wote.^f **11** Kwa maana kila mtu anayejiinua atanyenyekezwa, na yeyote anayejinyenyekeza atainuliwa.”^g

12 Kisha akamwambia yule mtu aliyemwalika: “Unapoa ndaa mlo wa mchana au wa jioni, usiwaite rafiki zako, ndugu

14:2 *Uvimbe unaosababishwa na umajimaji kongezeka mwilini.

zako, watu wako wa ukoo, au jirani zako walio matajiri. Huenda wao pia wakakualika, na hivyo kukulipa ulichowafanyia. **13** Lakini unapoa ndaa karamu, waalike maskini, viwete, vilema, na vipofu;^a **14** nawe utakuwa mwenye furaha, kwa sababu hawana kitu cha kukulipa. Kwa maana utalipwa katika ufufuo^b wa waadilifu.”

15 Aliposikia mambo hayo, mmoja wa wageni akamwambia: “Mwenye furaha ni yule anayekula* katika Ufalme wa Mungu.”

16 Yesu akamwambia: “Mtu fulani alikuwa akiandaa mlo mkubwa wa jioni,^c naye akawaalika watu wengi. **17** Saa ya mlo wa jioni ilipofika, akamtuma mtumwa wake awambie walioalikwa, ‘Njooni, kwa sababu kila kitu kiko tayari.’ **18** Lakini wote wakaaanza kutoa visingizio.^d Mmoja akasema, ‘Nilinunua shamba, ninahitaji kwenda kuliona; tafadhali, niwie radhi.’ **19** Mwingine akasema, ‘Nime-nunua jozi tano za ng’ombe,* ninaenda kuwakagua; tafadhali, niwie radhi.’^e **20** Na bado mwingine akasema, ‘Nimetoka tu kuoa, kwa hiyo siwezi kuja.’ **21** Basi yule mtumwa akarudi na kumwambia bwana wake mambo hayo. Kisha yule bwana wa nyumba akakasirika na kumwambia mtumwa wake, ‘Nenda upesi kwenye barabara kuu na vichocho vya jiji, uwalete maskini, viwete, vipofu, na vilema.’ **22** Baada ya muda yule mtumwa akasema, ‘Bwana, ni-

14:15 *Tnn., “anayekula mkate.” **14:19** *Au “ng’ombe kumi.”

SURA YA 14

a Ayu 31:16, 22
Met 3:27, 28

b Yoh 5:28, 29
Yoh 11:24
Mdo 24:15

c Mt 22:2

d Mt 22:3

e Mt 22:5

Safu ya 2

a Mt 22:9, 10

b Mt 21:43
Mt 22:8

c Ufu 12:11

d Mt 10:37
Lu 18:29, 30
Yoh 12:25

e Mt 16:24
Mk 8:34
Lu 9:23

mefanya ulivyoniagiza, lakini bado kuna nafasi.’ **23** Basi yule bwana akamwambia mtumwa, ‘Nenda barabarani na kwenye vijija uwahimize watu waje, ili nyumba yangu ijae.’^a **24** Kwa maana ninawaambia, hakuna hata mmoja wa watu waliokuwa wamealikwa atakayeonja mlo wangu wa jioni.”^b

25 Basi Yesu alikuwa akisafiri pamoja na umati mkubwa, kisha akageuka na kuwambia: **26** “Yeyote akija kwangu naye hamchukii* baba yake na mama yake na mke wake na watoto wake na ndugu na dada zake, ndiyo, hata uhai wake^c mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.^d **27** Yeyote asipouchukua mti wake wa mateso* na kuni-fuata hawezi kuwa mwanafunzi wangu.^e **28** Kwa mfano, ni nani kati yenu anayetaka kujenga mnara ambaye hakezi kwanza na kuhesabu gharama, ili aone kama ana kiasi cha kutosha kuukamilisha? **29** La sivyo, ataweka msingi lakini ashindwe kumaliza, na wote wanaomtazama wataanza kumdhihaki, **30** wakisema: ‘Mtu huyu alianza kujenga lakini akashindwa kumaliza.’ **31** Au mfalme akienda kupigana vita na mfalme mwingine, je, haketi kwanza na kufikiri iwapo akiwa na wanajeshi 10,000 anaweza kumshinda yule anayekuja akiwa na wanajeshi 20,000? **32** Ikiwa hawezi, basi yule mfalme mwingine akiwa bado yuko mbali sana, yeye huwatumia maba-

14:26 *Au “hampendi kwa kiwango kidogo zaidi.” *Au “nafsi yake.” **14:27** *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mti wa mateso.”

lozi ili kufanya amani. **33** Vivyo hivyo, kwa hakika yeyote kati yenu asipoaga* mali zake zote hawezi kuwa mwanafunzi wangu.^a

34 “Kwa kweli chumvi ni nzuri. Lakini ikipoteza nguvu yake, itakolezwa na nini?^b

35 Haifai kuchanganywa na udongo wala mbolea. Watu huitupa nje. Yule aliye na masikio ya kusikiliza na asikilize.”^c

15 Basi wakusanya kodi wote na watenda dhambi walikuwa wakikusanyika karibu naye ili kumsikiliza.^d **2** Mafarisayo na waandishi wakaendelea kunung'unika wakisema: “Mtu huyu huwakaribisha watenda dhambi na kula pamoja nao.”

3 Ndipo akawaambia mfano huu: **4** “Ikiwa mmoja wenu ana kondoo 100, naye ampo-teze mmoja, je, hatawaacha wale 99 nyikani aende kumtafuta yule aliyepotea mpaka ampate?^e **5** Na baada ya kumpata, anambeba mabegani na kushangilia. **6** Na anapofika nyumbani anawaita rafiki zake na jirani zake, na kuwaambia, ‘Shangilieni pamoja nami, kwa kuwa nimempata kondoo wangu aliyekuwa amepotea.’^f **7** Vivyo hivyo, ninawaambia kwamba kutakuwa na shangwe nyingi mbinguni kwa sababu ya mtenda dhambi mmoja anayetubu^g kuliko kwa waadilifu 99 ambao hawahitaji kutubu.

8 “Au mwanamke aliye na sarafu kumi za drakma* aki-poteza drakma[#] moja, je, ha-

14:33 *Au “asipoacha.” 15:8 *Angalia Nyongeza B14. 15:8, 9 #Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 14

a Mt 19:27
Lu 9:62
Flp 3:7, 8

b Mt 5:13
Mk 9:50
Kol 4:6

c Mt 13:43
Mk 4:9
Ufu 2:29

SURA YA 15

d Mt 9:10, 11
Mk 2:15, 16
Lu 5:29, 30
1Ti 1:15

e Eze 34:11, 16
Mt 18:12, 13
Lu 19:10

f Mt 18:14
Ro 12:15
1Pe 2:25

g Eze 33:11
Lu 5:32

Safu ya 2

a Mt 9:13
Mk 2:17

b Law 11:7, 8

tawasha taa, afagie nyumba yake na kuitafuta kwa maki-ni mpaka aipate? **9** Na baada ya kuipata, anawaita rafiki zake* na jirani zake na kuwaambia, ‘Shangilieni pamoja nami, kwa kuwa nimeipata sarafu ya drakma[#] niliyokuwa nimepoteza.’ **10** Vivyo hivyo, ninawaambia kwamba malaika wa Mungu hushangilia mtenda dhambi mmoja anapotubu.”^a

11 Kisha akasema: “Mtu fulani alikuwa na wana wawili. **12** Yule mdogo akamwambia baba yake, ‘Baba, nipe sehemu ya urithi ambayo ni yangu.’ Basi akawagawia wana-we mali yake. **13** Baada ya siku chache, yule mwana mdogo akakusanya vitu vyake vyote akasafiri kwenda nchi ya mbali, akiwa huko akatumia vibaya mali yake kwa kuishi maisha ya anasa.* **14** Alipokuwa ametumia kila kitu, njaa kali sana ikatokea katika nchi hiyo yote, naye hakuwa na chochote. **15** Hata alienda kuajiriwa na raia mmoja wa nchi hiyo, ambaye alimpeleka kwenye mashamba yake akalishie nguruwe.^b **16** Naye alitamani kujishibisha kwa maganda ya karuba ambayo nguruwe walikuwa wakila, lakini hakuna mtu aliyempa chochote.

17 “Aliporudiwa na fahamu akasema, ‘Baba yangu amejiri wafanyakazi wengi nao wana mkate kwa wingi, lakini mimi ninakufa njaa! **18** Nita-funga safari kwenda kwa baba yangu na kumwambia:

15:9 *Au “wanawake ambao ni rafiki zake.” 15:13 *Au “upotovu; bila kujali.”

“Baba, nimetenda dhambi dhidi ya mbingu na dhidi yako. **19** Sistahili tena kuitwa mwanao. Naomba niwe mmoja wa wafanyakazi wako.” **20** Basi akaondoka na kwenda kwa baba yake. Akiwa mbali, baba yake akamwona na kumsikiti-
kia, akakimbia, akamkumbatia* na kumbusu kwa wororo. **21** Kisha yule mwana akamwambia, ‘Baba, nimetenda dhambi dhidi ya mbingu na dhidi yako.’^a Sistahili tena kuitwa mwanao.’ **22** Lakini baba yake akawaambia watumwa, ‘Leteni upesi kanzu bora zaidi na kumvika, pia mvisheni pete mkononi na viatu miguuni. **23** Vilevile, leteni ndama aliyenoneshwa, mchinjeni, nasi tule na tusherehekee, **24** kwa sababu huyu mwanangu alikuwa amekufa na sasa yuko hai;’^b alikuwa amepotea naye amepatikana.’ Basi wakaanza kusherehekea.

25 “Sasa mwanawe mku-bwa alikuwa shambani, alipokuwa akirudi na kukaribia nyumba, akasikia sauti ya muziki na dansi. **26** Basi akamwita mtumishi mmoja akamuuliza kilichokuwa kikiendelea. **27** Akamjibu, ‘Ndugu yako amerudi, kwa hiyo baba yako amechinja ndama aliyenoneshwa kwa sababu amerudi akiwa na afya njema.’” **28** Lakini akakasirika na kukataa kuingia ndani. Basi baba yake akatoka nje akaanza kumbembeleza. **29** Akamjibu baba yake, ‘Tazama! nimekutumikia kwa

15:20 *Tnn., “akamwangukia shingoni.”
15:27 *Au “amerudi salama.”

SURA YA 15

a 2Nya 7:14
Zb 32:5
Zb 51:4
Met 28:13
Lu 18:13
1Yo 1:9

miaka mingi na sijawahi kuvunja amri yako hata mara moja, lakini hujawahi kunipa hata mara moja mwanambuzi ili nijifurahishe pamoja na rafiki zangu. **30** Lakini mara tu alipofika huyu mwanao aliyetumia vibaya* mali yako na makahaba, ulimchinja ndama aliyenoneshwa.’ **31** Baba yake akamjibu, ‘Mwanangu, umekuwa pamoja nami siku-zote, na vitu vyangu vyote ni vyako. **32** Lakini ilibidi tusherehekee na kushangilia, kwa maana ndugu yako alikuwa amekufa lakini sasa yuko hai; alikuwa amepotea naye amepatikana.”

16 Pia, Yesu akawaambia wanafunzi wake: “Tajiri fulani alikuwa na msimamizi* ambaye alishtakiwa kwamba anatomia vibaya mali yake. **2** Basi akamwita na kumwambia, ‘Ni mambo gani haya ninayosikia kukuhusu? Lete rekodi za usimamizi kwa sababu huwezi tena kusimamia nyumba yangu.’ **3** Kisha yule msimamizi akajiambia, ‘Nita-fanya nini kwa kuwa bwana wangu ananiondoa kazini? Sina nguvu za kulima na ninaona aibu kuombaomba. **4** Aha! Najua nitakachofanya, ili nitakapoachishwa kazi, watu wanikaribishe nyumbani mwao.’ **5** Akawaita mmoja mmoja wale waliokuwa na madeni ya bwana wake, akamuuliza wa kwanza, ‘Unadaiwa kiasi gani na bwana wangu?’ **6** Akajibu, ‘Vipimo* 100 vya

15:30 *Tnn., “aliyekula; aliyeharibu.”
16:1 *Au “msimamizi wa nyumba.”
16:6 *Au “vipimo vya bathi.” Bathi moja ilikuwa sawa na lita 22. Angalia Nyongeza B14.

b Ro 6:13
Efe 2:4, 5

mafuta ya zeituni.’ Akamwambia, ‘Chukua hati yako ya mapatano, uketi na upepsi uandike 50.’ **7** Kisha akamuuliza mwingine, ‘Na wewe, unadaiwa kiasi gani?’ Akasema, ‘Vipimo vikubwa 100* vya ngano.’ Akamwambia, ‘Chukua hati yako ya mapatano uandike 80.’ **8** Bwana wake akamsifu yule msimamizi kwa sababu ingawa hakuwa mwadilifu, alitenda kwa hekima inayotumika,* kwa maana wana wa mfumo huu wa mambo[#] wana hekima zaidi katika kizazi chao kuliko waliavyo wana wa nuru.^a

9 “Pia, ninawaambia: Jifanyieni marafiki kupitia mali zisizo za uadilifu,^b ili zitakapokwisha wawapokee katika makao ya milele.^c **10** Mtu aliye mwaminifu katika lililo dogo ni mwaminifu katika lililo kubwa pia, na mtu asiye mwaminifu katika lililo dogo si mwaminifu katika lililo kubwa pia. **11** Kwa hiyo, msipokuwa waaminifu kuhusu mali zisizo za uadilifu, ni nani atakayewakabidhi kilicho cha kweli? **12** Na msipokuwa waaminifu kuhusu mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa mali yenu wenyewe?^d **13** Hakuna mtumishi anayeweza kuwatumikia mabwana wawili, kwa maana atamchukia mmoja na kumpenda mwingine, au atashikamana na mmoja na kumdharau mwingine. Hamwezi

16:7 *Au “vipimo 100 vya kori.” Kori moja ilikuwa sawa na kilogramu 170. Angalia Nyongeza B14. **16:8** *Au “kwa busara; kwa werevu.” [#]Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mfumo wa mambo.”

SURA YA 16

a Yoh 12:36
Efe 5:8
1Th 5:5

b Mt 19:21
1Ti 6:17

c Mt 25:34
Lu 12:20, 21

d Lu 12:48

Safu ya 2

a Mt 6:24

b Isa 53:3

c Mt 6:2
Mt 23:27, 28
Lu 18:9

d Isa 16:7
1Nya 28:9
2Nya 6:30

e 1Pe 5:5

f Mt 11:12, 13

g Mt 5:17, 18

h Mt 5:32
Mt 19:9
Mk 10:11, 12

kuwa watumwa wa Mungu na wa Utajiri.”^a

14 Sasa Mafarisayo, waliopenda pesa, walikuwa wakisikiliza mambo hayo yote, nao wakaanza kumdhihakiki.^b

15 Basi akawaambia: “Mnaji-tangaza kuwa waadilifu mbele ya wanadamu,^c lakini Mungu anaijua mioyo yenu.^d Kwa maana kitu kinachoheshimiwa sana na wanadamu kinamchukiza Mungu.^e

16 “Sheria na Manabii walikuwa mpaka Yohana. Tangu wakati huo habari njema za Ufalme wa Mungu zinatangazwa, na watu wa namna zote wanajitahidi kuufikia.^f **17** Kwa kweli, ni rahisi zaidi kwa mbingu na dunia kupitilia mbali kuliko sehemu yoyote ya herufi ya Sheria kukaosa kutimia.^g

18 “Kila mtu anayempa talaka mke wake na kuoa mwingine anafanya uzinzi, na yeye anayemwoa mwanamke aliyepewa talaka na mumewe anafanya uzinzi.^h

19 “Kulikuwa na tajiri ambaye alikuwa akivaa mavazi ya zambarau na kitani, na alifurahia maisha ya kifahari siku kwa siku. **20** Lakini mtu fulani aliyekuwa akiombaomba aliyetitwa Lazaro, alikuwa akiletwa kwenye lango lake. Alikuwa na vidonda mwili mzima, **21** naye alikuwa akitamani kula mabaki yaliyoanguka kutoka kwenye meza ya yule tajiri. Ndiyo, pia, mbwa walikuwa wakija na kuramba vidonda vya ke. **22** Baada ya muda yule mtu aliyekuwa akiombaomba akafa, malaika wakambeba

na kumpeleka kando ya Abrahamu.*

“Pia, yule tajiri akafa na kuzikwa. **23** Akiwa Kaburini* akatazama juu, akiteseka sana, akamwona Abrahamu kwa mbali na Lazaro akiwa kando yake.[#] **24** Kwa hiyo akamwita, ‘Baba Abrahamu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake katika maji au poze ulimi wangu, kwa maana ninateseka sana katika moto huu mkali.’ **25** Lakini Abrahamu akamwambia, ‘Mwanangu, kumbuka wewe ulikuwa na vitu vingi vizuri maishani, naye Lazaro aliteseka sana. Hata hivyo, sasa anafarijika lakini wewe unateseka. **26** Isitoshe, kuna shimo kubwa kati yetu nanyi, hivi kwamba wale wanaotaka kuvuka kutoka hapa kuja kwenye hawawezi, wala watu hawawezi kuvuka kutoka huko na kuja kwetu.’ **27** Kisha akasema, ‘Basi kama ni hivyo ninakuomba, baba, umtume kwenye nyumba ya baba yangu, **28** ili awatolee ushahidi kamili ndugu zangu watano wasije wakaingia mahali hapa pamaateso.’ **29** Lakini Abrahamu akasema, ‘Wana Musa na Manabii; waache wawasikilize hao.’^a **30** Kisha akasema, ‘Hapana, Baba Abrahamu, hawatasikiliza, lakini mtu fulani kutoka kwa wafu akienda kwao, watatubu.’ **31** Lakini akamwambia, ‘Kama hawamsikilizi Musa^b na Manabii,

16:22 *Tnn., “kwenye kifua cha Abrahamu.” 16:23 *Au “Hadesi.” Angalia Kamusi, uku. 2012. #Tnn., “kwenye kifua chake.”

SURA YA 16

a Kum 18:18
Lu 24:25-27

b Yoh 5:46

Safu ya 2

SURA YA 17

a Mt 18:6
Mk 9:42

b Met 17:10

c Law 19:17
Mt 18:15

d Isa 55:7
Mt 6:12
Mt 18:21, 22
Kol 3:13
1Pe 4:8

e Mk 9:23, 24
Ebr 12:2

f Mt 17:20
Mt 21:21
Mk 11:23

hawataamini hata mtu fulani akifufuliwa kutoka kwa wafu.”

17 Ndipo akawaambia wanafunzi wake: “Lazima vikwazo vije. Hata hivyo, ole wake mtu atakayervisababisha! **2** Ingekuwa afadhali kwake kama angefungiwa shingoni jiwe la kusagia kisha atupwe baharini kuliko amkwaze mmoja wa hawa wadogo.^a **3** Jiangalieni ninyi wenyewe. Ndugu yako akite nda dhambi mkeme,^b na akitubu, msamehe.^c **4** Hata akitutendea dhambi mara saba kwa siku, naye anarudi kwako mara saba akisema, ‘ninatubu,’ unapaswa kumsamehe.”^d

5 Mitume wakamwambia Bwana: “Tusaidie tuwe na imani zaidi.”^e **6** Bwana akasema: “Kama mngekuwa na imani inayolingana na mbegu ya haradali, mngeuambia mti huu wa mforsadi, ‘Ng’oka ukapandwe baharini!’ nao unge-watii.”^f

7 “Ni nani kati yenu aliye na mtumwa anayelima shamba au kuchunga wanyama, ambaye akirudi kutoka shambani, atamwambia ‘Njoo upesi, keti ule chakula?’ **8** Hapana. Badala yake atamwambia, ‘Nitayarishie chakula cha jioni, na ujifunge vazi la kazi ili unihudumie mpaka nitakapomaliza kula na kunywa, kisha unaweza kula na kunywa.’ **9** Je, utamshukuru mtumwa huyo kwa sababu alifanya mambo uliyomwagiza? **10** Vivyo hivyo, baada ya kufanya mambo mliyoagizwa, semeni: ‘Sisi ni watumwa wasiofaa kitu. Tu-

mefanya kile tulichopaswa kufanya.”^a

11 Alipokuwa akienda Yerusalem, alipita kati ya Samaria na Galilaya. **12** Alipokuwa akiingia katika kijiji fulani alikutana na wanaume kumi wenye ukoma, lakini walisimama mbali naye.^b **13** Kisha wakasema kwa sauti kubwa: “Yesu, Mwalimu, tuhurumie!”^c **14** Alipowaona, akawaambia: “Nendeni mka-jionyeshe kwa makuhani.”^c Basi walipokuwa wakienda wakatakaswa.^d **15** Mmoja wao alipoona amepona, akarudi akimtukuza Mungu kwa sauti kubwa. **16** Akaa-nguka kifudifudi miguuni pa Yesu na kumshukuru. Isitoshe, alikuwa Msamaria.^e **17** Yesu akauliza: “Wote kumi walitakaswa, sivyo? Basi, wako wapi wale wengine tisa? **18** Je, hakuna mwingine aliyerudi ili kumtukuza Mungu isipokuwa mtu huyu wa taifa lingine?” **19** Kisha akamwambia: “Simama uende; imani yako imekuponya.”^f

20 Mafarisayo walipomuuliza Ufalme wa Mungu utakuja lini,^g aliwajibu: “Ufalme wa Mungu hautakuja ukionekana waziwazi; **21** wala watu hawatasema, ‘Tazama! uko hapa!’ au, ‘Uko pale!’ Kwa maana tazama! Ufalme wa Mungu uko katikati yenu.”^h

22 Kisha akawaambia wanafunzi: “Siku zitafika ambapo mtatamani kuona moja kati ya siku za Mwana wa binadamu lakini hamtaiona. **23** Na watu watawaambia, ‘Angalia

17:13 *Au “tuonyeshe rehema!” 17:21 *Au “uko miongoni mwenu.”

SURA YA 17

a 1Ko 9:16

b Law 13:45, 46

c Law 14:2-4
Kum 24:8
Mt 8:3, 4
Lu 5:13, 14

d 2Fa 5:1, 14

e 2Fa 17:24
Yoh 4:9

f Mt 9:22
Mk 5:34
Lu 7:50

g Mt 24:3

h Mt 12:28
Mt 21:5

Safu ya 2

a Mt 24:23
Mk 13:21
Lu 21:8
1Yo 4:1

b Da 7:13

c Mt 24:27

d Mk 8:31
Mk 9:31
Lu 9:22

e Mwa 6:5

f Mt 24:37-39

g Mwa 7:7

h Mwa 7:17, 21

i Mwa 19:15

j Mwa 19:24, 25

k 1Ko 1:7
2Th 1:7, 8

l Mwa 19:17, 26

m Mt 10:39
Mt 16:25
Mk 8:35
Lu 9:24
Yoh 12:25

pale!’ au, ‘Angalia hapa!’ Msiende wala msiwafuate.”^a

24 Kwa maana kama radi inavyong’aa kutoka sehemu moja ya mbingu mpaka sehemu nyingine, ndivyo Mwana wa binadamu^b itakavyokuwa katika siku yake.^c **25** Hata hivyo, kwanza lazima apatwe na mateso mengi na kukataliwa na kizazi hiki.^d **26** Isitoshe, kama ilivyokuwa katika siku za Noa,^e ndivyo itakavyokuwa katika siku za Mwana wa binadamu:^f **27** walikuwa wakila, walikuwa wakinywa, wanaume walikuwa wakioa na wanawake wakiolewa, mpaka siku ambayo Noa aliingia ndani ya safina,^g na Gharika ikaja na kuwaangamiza wote.^h **28** Vivyo hivyo, kama ilivyokuwa katika siku za Loti:ⁱ walikuwa wakila, walikuwa wakinywa, walikuwa wakinunua, walikuwa wakiuza, walikuwa wakipanda, na walikuwa wakijenga. **29** Lakini siku ambayo Loti alitoka Sodoma, kulinyesha mvua ya moto na kiberiti kutoka mbinguni na wote wakaa-ngamizwa.^j **30** Ndivyo itakavyokuwa siku ambayo Mwana wa binadamu atafunuliwa.^k

31 “Siku hiyo mtu aliye kwenye paa la nyumba asishuke kuchukua mali iliyo ndani ya nyumba yake, vivyo hivyo mtu aliye shambani, asirudi kwenye vitu vilivyo nyuma. **32** Mkumbukeni mke wa Loti.^l **33** Yeyote anayetaka kuuokoa uhai wake* ataupoteza, lakini yeyote anayeupoteza atauokoa.^m **34** Ninawaambia, usiku huo watu wawili watakuwa katika kitanda kimoja;

17:33 *Au “nafsi yake.”

mmoja atachukuliwa, lakini mwingine ataachwa.^a **35** Wanawake wawili watakuwa wakisaga kwenye jiwe moja la kusagia; mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa.” **36** *—**37** Basi wakamuuliza: “Wapi, Bwana?” Akawajibu: “Mahali palipo na mzoga, hapo ndipo tai watakapokusanyika.”^b

18 Kisha akawaambia mfanono ili kuwaonyesha umuhimu wa kuendelea kusali bila kukata tamaa.^c **2** Akasema: “Katika jiji fulani kulikuwa na mwamuzi ambaye hakumwogopa Mungu wala hakumheshimu mtu yeyote. **3** Pia, katika jiji hilo kulikuwa na mjane ambaye alikuwa akienda kwake na kumwomba, ‘Hakikisha kwamba kesi yangu itaamuliwa kwa haki.’ **4** Kwa muda fulani yule mwamuzi alikataa, lakini baadaye akajiambia, ‘Ingawa simwogopi Mungu wala simheshimu mtu yeyote, **5** kwa sababu huyu mjane anaendelea kunisumbua, nitahakikisha amepata haki ili asiendele kuja kunichosha na maombi yake.’”^d **6** Kisha Bwana akasema: “Sikieni alichosema mwamuzi huyo ingawa si mwadilifu! **7** Kwa hakika, je, Mungu hatawatendea haki watu wake waliochaguliwa ambao wanamlilia mchana na usiku,^e huku akiwaonyesha subira?^f **8** Ninawaambia, atawatendea haki upesi. Hata hivyo, Mwana wa binadamu atakapofika, je, kweli ataipata imani hii* duniani?”

17:36 *Angalia Nyongeza A3. 18:5 *Au “kunishambulia mpaka animalize.” 18:8 *Au “imani kama hii.” Tnn., “ile imani.”

SURA YA 17

a Mt 24:40, 41

b Mt 24:28

SURA YA 18

c Ro 12:12
Efe 6:18
Flp 4:6
Kol 4:2
1Th 5:17

d Lu 11:7, 8

e Ufu 6:9,10

f 2Pe 3:9

Safu ya 2

a Mt 23:23

b Zb 51:1-3

c Isa 66:2
Mt 21:28-31

d Isa 2:11
Mt 23:12
Yak 4:6
1Pe 5:5

e Mt 19:13-15
Mk 10:13-16

f 1Pe 2:2

g Mt 18:3
Mk 10:15

9 Pia, aliwaambia mfano huu wale waliojiona kuwa waadilifu na kuwadharau wengine: **10** “Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja alikuwa Farisayo na mwingine mkusanya kodi. **11** Yule Farisayo akasimama na kuanza kusali akisema moyoni, ‘Ee Mungu, ninakushukuru kwa sababu mimi si kama watu wengine—wanyang’anyi, wasio waadilifu, wazinzi—au hata kama mkusanya kodi huyu. **12** Mimi hufunga mara mbili kwa juma; ninatoa sehemu ya kumi ya mapato yangu yote.’^a **13** Lakini yule mkusanya kodi alikuwa amesimama mbali kidogo na hata hakutaka kutazama mbinguni, bali alijipigapiga kifurusi akisema, ‘Ee Mungu, nihurumie* mimi mtenda dhambi.’^b **14** Ninawaambia, mtu huyu alishuka kwenda nyumbani akiwa mwadilifu mbele za Mungu kuliko yule Farisayo.^c Kwa sababu kila mtu anayejiinua atafedheheshwa, lakini yeyote anayejiyenyekeza atainuliwa.”^d

15 Sasa watu wakamletea Yesu watoto wao wadogo ili awaguse, lakini wanafunzi walipoona hivyo wakaanza kuwakemea.^e **16** Lakini Yesu akawaita wale watoto, akisema: “Waacheni watoto wadogo waje kwangu, na msijaribu kuwazuia, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa wale walio kama wao.^f **17** Kwa kweli ninawaambia, yeyote asiyeupokea Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hataingia kamwe ndani yake.”^g

18:13 *Au “nionyeshe rehema.”

18 Mtawala fulani akamuuliza: “Mwalimu Mwema, ninapaswa kufanya nini ili niurithi uzima wa milele?”^a

19 Yesu akamwambia: “Kwa nini unaniita mwema? Hakuna aliye mwema, isipokuwa mmoja, Mungu.”^b **20** Unazijua amri hizi: ‘Usifanye uzinzi,^c usiue,^d usiibe,^e usitoe ushahidi wa uwongo,^f mheshimu baba yako na mama yako.’”^g **21** Ndipo akasema: “Nimeyashika hayo yote tangu nilipokuwa kijana.” **22** Baada ya kusikia hilo, Yesu akamwambia, “Bado kuna jambo unalokosa: Uza kila kitu ulicho nacho na uwagawie maskini pesa hizo, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha uje uwe mfuasi wangu.”^h

23 Aliposikia hivyo, akahuzunika sana, kwa sababu alikuwa tajiri sana.ⁱ

24 Yesu akamtazama na kusema: “Itakuwa vigumu sana kwa wale walio na pesa kuingia katika Ufalme wa Mungu!” **25** Kwa kweli, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano ya kushonea kuliko tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu.”^k

26 Wale waliosikia hilo waukauliza: “Ni nani anayeweza kuokolewa?”^l **27** Akasema: “Mambo yasiyowezekana kwa wanadamu yanawezekana kwa Mungu.”^m **28** Lakini Petro akamwambia: “Tazama! Tumeacha vitu vyetu na kukufuata.”ⁿ **29** Akawaambia: “Kwa kweli ninawaambia, hakuna yeyote ambaye ameaacha nyumba, au mke, au ndugu, au wazazi, au watoto kwa ajili ya Ufalme wa Mungu”

SURA YA 18

a Mt 19:16-22
Mk 10:17-22
Lu 10:25-28

b Mt 19:17
Mk 10:18

c Kut 20:14
Kum 5:18

d Kut 20:13
Kum 5:17

e Kut 20:15
Kum 5:19

f Kut 20:16
Kum 5:20

g Kut 20:12
Kum 5:16
Ro 13:9
Efe 6:2

h Mt 6:20
Mt 19:21
Mk 10:21
Lu 12:33
ITI 6:18, 19

i Mt 19:22
Mk 10:22

j Met 11:28
Mt 19:23
Mk 10:23, 24
ITI 6:9

k Mt 19:24
Mk 10:25

l Mt 19:25

m Mt 19:26
Mk 10:27

n Mt 19:27

o Mt 19:28, 29
Mk 10:29, 30

Safu ya 2

a Ufu 2:10

b Mt 16:21
Mt 20:17-19
Mk 10:32-34

c Mt 27:2
Mdo 3:13

d Zb 22:7

e Isa 50:6

f Isa 53:5, 7

g Mk 10:33, 34
Lu 9:22

h Mt 20:29-34
Mk 10:46-52

30 ambaye hatapata mara nyingi zaidi wakati huu, na katika mfumo wa mambo* unaojua, uzima wa milele.”^a

31 Ndipo akawaita kando wale 12 na kuwaambia: “Tazama! Tunapanda kwenda Yerusalem, na mambo yote yaliyoandikwa kupitia manabii kuhusu Mwana wa binadamu yatatimia.”^b **32** Kwa mfano, atatiwa mikononi mwa watu wa mataifa^c naye atadhihakiwa,^d atatendewa kwa dharau, na kutemewa mate.^e **33** Watampiga mijeledi, kisha watamuua,^f lakini siku ya tatu atafufuka.”^g **34** Hata hivyo, hawakuelewa maana ya mambo hayo, kwa sababu walikuwa wamefichwa maneno hayo, nao hawakuelewa mambo yaliyosemwa.

35 Yesu alipokaribia Yeriko kipofu mmoja alikuwa ameketi kando ya barabara akiombaoomba.^h **36** Aliposikia umati ukipita, akaanza kuuliza kili-chokuwa kikiendelea. **37** Wakamjibu: “Yesu Mnazareti ndiye anayepita!” **38** Ndipo akasema kwa sauti kubwa: “Yesu, Mwana wa Daudi, ni hurumie!”* **39** Wale waliokuwa mbebe wakaanza kumkemea wakimwambia anyamaze, lakini akazidi kusema kwa sauti kubwa: “Mwana wa Daudi, ni hurumie!”* **40** Kisha Yesu akasimama na kuagiza mtu huyo aletwe kwake. Alipokaribia, Yesu akamuuliza: **41** “Unataka nikufanyie nini?” Akasema: “Bwana, nao mba niweze kuona tena.”

18:30 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

18:31 *Au “yatakamilika.” **18:38, 39**

*Au “nionyeshe rehema!”

42 Basi Yesu akamwambia: "Ona tena; imani yako imeku-ponya."^a **43** Mara moja akaanza kuona tena, naye akaanza kumfuata Yesu^b huku akimtu-kuza Mungu. Pia, watu wote walipoona hayo, wakamsifu Mungu.^c

19 Yesu akaingia Yeriko, naye alikuwa akipita kati-ka jiji hilo. **2** Kulikuwa na mwanamume aliyelitwa Zaka-yo; alikuwa mkuu wa waku-sanya kodi, na alikuwa taji-ri. **3** Basi, alitamani sana kumwona Yesu, lakini ha-kuweza kwa sababu ya uma-ti, kwa maana alikuwa mfupi. **4** Basi akakimbia mbele na kupanda juu ya mti wa mkuyu* ili amwone Yesu, kwa maana alikuwa karibu kupitia njia hiyo. **5** Yesu alipofika hapo, akatazama juu akamwambia: "Zakayo, shu-ka haraka, kwa maana leo la-zima nikae nyumbani kwako." **6** Basi akashuka haraka na kumkaribisha kwa shangwe awe mgeni wake. **7** Wote walipoona hivyo, wakaanza kunung'unika wakisema: "Amee-nda kumtembelea mtenda dhambi."^d **8** Lakini Zakayo akasimama na kumwambia Bwana: "Tazama! Nitawapa maskini nusu ya mali za-angu, Bwana, na chochote nilichomnyang'anya mtu,* ni-tamrudishia mara nne."^e **9** Ndipo Yesu akamwambia: "Leo wokovu umekuwa katika nyumba hii, kwa sababu yeye pia ni mwana wa Abrahamu. **10** Kwa maana Mwana wa bi-

19:4 *Au "mforsadi-tini." **19:8** *Au "nilichomnyang'anya kwa shtaka la uwongo."

SURA YA 18

a Lu 7:50
Lu 17:19

b Mt 20:34

c Lu 5:26

SURA YA 19

d Mt 9:11
Lu 5:30
Lu 15:2

e Kut 22:1
Law 6:4, 5

Safu ya 2

a Eze 34:16
Mt 9:13
Mt 15:24
Lu 15:4
Ro 5:8
ITI 1:15

b Mdo 1:6

c Mt 25:14
Mk 13:34
Yoh 18:36

d Mt 25:15

e Mt 25:19

f Mt 25:20, 21

g Lu 16:10

h Mt 25:22, 23

nadamu alikuja kutafuta na kuokoa kilichopotea."^a

11 Walipokuwa wakisikili-za mambo hayo, akawaambia mfano mwingine, kwa saba-bu alikuwa karibu na Yeru-salemu nao walifikiri Ufalme wa Mungu ungetokea ghafla.^b

12 Basi akasema: "Mtu fulani wa familia mashuhuri alitaka kusafiri kwenda nchi ya mbali^c ili apokee mamlaka ya kifal-me kisha arudi. **13** Akawaita kumi kati ya watumwa wake akawapa mina* kumi na ku-waambia, 'Fanyeni nazo bia-shara mpaka nitakaporudi.'^d

14 Lakini raia zake wali-mchukia, nao wakatuma ma-balozi wamfuate na kusema, 'Hatutaki mtu huyu awe mfal-me wetu.'

15 "Mwishowe aliporudi ba-ada ya kupokea mamlaka ya kifalme,* aliwaita watumwa aliokuwa amewapa pesa,[#] ili ajue faida waliyopata kwa ku-fanya biashara.^e **16** Basi wa kwanza akaja na kusema, 'Bwana, mina yako moja imeleta faida ya mina kumi.'^f

17 Akamwambia, 'Umefanya vema, mtumwa mwema! Kwa kuwa umekuwa mwaminifu katika jambo dogo sana, uta-tawala majiji kumi.'^g **18** Ki-sha wa pili akaja na ku-sema, 'Bwana, mina yako moja, imeleta faida ya mina tano.'^h **19** Vilevile akamwa-mbia, 'Wewe pia, utatawala majiji matano.' **20** Lakini mwingine akaja, akasema, 'Bwana, hii hapa mina yako,

19:13 *Mina ya Ugiriki ilikuwa na uzi-to wa gramu 340 na ilikuwa na thamani ya drakma 100. Angalia Nyongeza B14. **19:15** *Au "ufalme." [#]Tnn., "fedha."

niliifunga kwa kitambaa nikai-ficha. **21** Nilikuogopa kwa sababu wewe ni mtu mkali; wewe huchukua kile ambacho hukuweka akiba, na kuvuna kile ambacho hukupanda.’^a **22** Akamwambia, ‘Ninakuhukumu kwa maneno yako mwenyewe, mtumwa mwovu. Uli-jua, sivyo, kwamba mimi ni mtu mkali, ambaye huchukua kile ambacho sikuweka akiba na kuvuna kile ambacho sikupanda?’^b **23** Basi kwa nini hukuziweka pesa* zangu benki? Kisha baada ya kurudi, ningezichukua zikiwa na faida.’

24 “Ndipo akawaambia wale waliokuwa wamesimama hapo, ‘Chukueni mina hiyo mka-mpe yule aliye na mina kumi.’^c **25** Lakini wakamwambia, ‘Bwana, tayari huyo ana mina kumi!’— **26** ‘Ninawaambia, kila mtu aliye na kitu, ataongezewa, lakini yule asiye na kitu, hata kile alichu nacho kitachukuliwa.’^d **27** Isitoshe, waleteni adui zangu ambao hawakutaka niwe mfalme wao, muwauwe mbele yangu.”

28 Baada ya Yesu kusema hayo, akapanda kuelekea Yerusalemu. **29** Alipokaribia Bethfage na Bethania kwenye Mlima wa Mizeituni,^e akawatuma wawili kati ya wanafunzi,^f **30** akisema: Nendeni katika kijiji mtakachokiona, na mtakapoingia mtamwona mwanapunda akiwa amefungua, ambaye hakuna mtu amewahi kuketi juu yake. Mfungu- eni na kumleta. **31** Lakini mtu akiwauliza, ‘Kwa nini mnamfungua?’ Mwa- mbieni, ‘Bwana anamhitaji.”

19:23 * Tnn., “fedha.”

SURA YA 19

a Mt 25:24

b Mt 25:26, 27

c Mt 25:28

d Mt 13:12
Mt 25:29
Mk 4:25
Lu 8:18

e Mdo 1:12

f Mt 21:1-3
Mk 11:1-6

Safu ya 2

a Mt 21:6, 7

b Zek 9:9
Mk 11:7-10
Yoh 12:14, 15

c Mt 21:8

d Zb 118:26
Mt 21:9
Mk 11:9

e Mt 21:15
Yoh 12:19

f Yoh 11:35

g Isa 6:9, 10
Mt 13:14

32 Basi wale waliotumwa wa-kaenda na kupata sawasawa na vile Yesu alivyowaambia.^a

33 Lakini walipokuwa waki-mfungua mwanapunda huyo, wenyewe wakawauliza: “Mbo-na mnamfungua huyo mwanapunda?” **34** Wakajibu: “Bwana anamhitaji.” **35** Wakampeleka kwa Yesu, nao wakaweka mavazi yao ya nje juu ya huyo mwanapunda na kumketisha Yesu juu yake.^b

36 Alipokuwa akienda wali-kuwa wakitandaza mavazi yao ya nje barabarani.^c **37** Alipokaribia tu barabara ya kushuka Mlima wa Mizeituni umati wote wa wanafunzi ukaanza kushangilia na kumsifu Mungu kwa sauti kubwa kwa sababu ya matendo yote yenye nguvu ambayo walikuwa wameona, **38** na kusema: “Amebarikiwa yule anayekuja akiwa Mfalme katika jina la Yehova!* Amani mbinguni, na utukufu katika vileye vilivyvo juu!”^d **39** Hata hivyo, baadhi ya Mafarisayo waliokuwa kwenye umati wakamwambia: “Mwalimu, wakemee wanafunzi wako.”^e **40** Lakini akajibu: “Ninawaambia, hata hawa wakinyamaza, mawe yata-paza sauti.”

41 Alipokaribia jiji la Yerusalemu, akalitazama na kulililia,^f **42** akisema: “Kama wewe, naam wewe, ungefahamua leo mambo yanayokuletea amani—lakini sasa yamefichwa kutoka machoni pako.^g **43** Kwa sababu siku zitakuja, adui zako watakapojenga ngome yenye miti iliyochongoka kukuzunguka,

19:38 * Angalia Nyongeza A5.

nao watakungira* kila upande.^a **44** Watakuangusha chini wewe na watoto wako walio ndani yako,^b nao hawataacha jiwe juu ya jiwe lingine,^c kwa sababu hukutambua wakati wa kukaguliwa kwako.”

45 Kisha akaingia hekaluni na kuanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza,^d **46** akiwaambia: “Imeandikwa, ‘Nyumba yangu itakuwa nyumba ya sala,’^e lakini mmeifanya kuwa pango la wanyang’anyi.”^f

47 Akaendelea kufundisha kila siku hekaluni. Lakini wakuu wa makuhani, waandishi na viongozi wa watu walikuwa wakitaka kumuua;^g **48** hata hivyo hawakufanikiwa, kwa maana watu wote walikuwa wakimfuata sana ili wamsikilize.^h

20 Siku moja alipokuwa akifundisha watu hekaluni na kutangaza habari nje-ma, wakuu wa makuhani, waandishi na wazee wakaja, **2** nao wakasema: “Tuambie, unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Au ni nani aliyekupa mamlaka hayo?”ⁱ **3** Akawajibu: “Mimi pia nitawauliza swali, nanyi mnijibu: **4** Je, ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?”^j **5** Wakaanza kujadiliana kati yao wakisema: “Tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’ atatuuliza, ‘Kwa nini hamku-mwamini?’ **6** Lakini tukisema, ‘Ulitoka kwa wanadamu,’ watu wote watatupiga mawe, kwa sababu wanaamini Yohana alikuwa nabii.”^k **7** Basi

19:43 *Au “watakutaabisha.” **20:4** *Au “chanzo chake ni wanadamu?”

SURA YA 19

a Kum 28:52
Da 9:26
Lu 21:20

b Lu 23:28, 29

c Mt 24:2
Mk 13:2
Lu 21:6

d Mt 21:12
Mk 11:15, 16

e Isa 56:7

f Yer 7:11
Mt 21:13
Mk 11:17
Yoh 2:16

g Mk 11:18

h Mk 12:37
Lu 21:38

SURA YA 20

i Mt 21:23-27
Mk 11:27-33

j Lu 7:29

Safu ya 2

a Isa 5:7

b Mt 21:33-41
Mk 12:1-9

c 2Fa 17:13, 14
2Nya 36:15, 16
Mdo 7:52
Ebr 11:36, 37

d Mt 17:5
Yoh 3:16

e Mdo 3:15

wakamjibu kwamba hawajui chanzo chake. **8** Yesu aka-waambia: “Nami siwaambii ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani.”

9 Yesu akaanza kuwaambia watu mfano huu: “Mtu fulani alipanda shamba la mizabibu^a akalikodisha kwa wakulima, kisha akasafiri kwenda ng’ambo, akakaa huko muda mrefu.^b **10** Majira yalipofika akamtuma mtumwa kwa wakulima ili wampe baadhii ya matunda ya shamba la mizabibu. Hata hivyo, wale wakulima wakampiga na kumfukuza mikono mitupu.^c **11** Lakini akamtuma mtumwa mwingine. Huyu pia wakampiga, wakamwaibisha,* na kumfukuza mikono mitupu. **12** Bado tena akamtuma wa tatu; huyo pia walimjeruhi na kumtupa nje. **13** Ndi-po mwenye shamba la mizabibu akasema, ‘Nifanye nini? Nitamtu mwanangu mpendwa.^d Labda watamheshimu.’ **14** Wakulima walipomwona wakaambiana, ‘Huyu ndiye mrithi. Basi tumuue, ili urithi wake uwe wetu.’ **15** Wakamtupa nje ya shamba la mizabibu na kumuua.^e Kwa hiyo, mwenye shamba la mizabibu atawafanya nini? **16** Atakuja na kuwaua wakulima hao, kisha atawapa watu wengine shamba hilo la mizabibu.”

Waliposikia hivyo wakasema: “Jambo hilo lisitukie kamwe!” **17** Lakini akawatazama moja kwa moja na kusema: “Basi, andiko hili linamaanisha nini: ‘Jiwe ambalo waje-

20:11 *Au “wakamvunjia heshima.”

nzi walilikataa, limekuwa jiwe kuu la pembeni'?^a **18** Kila mtu anayeanguka kwenye jiwe hilo atavunjika vipandevipande.^b Na litamponda yeyote litakayemwangukia."

19 Waandishi na wakuu wa makuhani walitambua kwa mba mfano aliosema uliwahusu, basi walitaka kumkamata saa hiyo hiyo, lakini waliwagopu watu.^c **20** Baada ya kumtazama kwa makini, wakatumu watu waliowakodi kisiri wajifanye kuwa waadilifu ili wamnase Yesu kwa maneno yake^d na kumkabidhi kwa serikali na kwa mamalaka ya gavana. **21** Nao wakamuuliza: "Mwalimu, tunajua wewe husema na kufundisha kwa usahihi na huna ubaguzi, bali unafundisha njia ya Mungu kupatana na kweli: **22** Je, ni halali* au si halali kwetu kumlipa Kaisari kod?" **23** Lakini alitambua ujanja wao na kuwaambia: **24** "Nionyesheni dinari.* Ina sura na maandishi ya nani?" Wakajibu: "Kaisari." **25** Akawaambia: "Basi mlipeni Kaisari^e vitu vya Kaisari, na Mungu vitu vya Mungu."^f **26** Kwa hiyo, wakashindwa kumnasa kwa maneno yake mbele ya watu, nao wakanyamaza wakiwa wameshangazwa na jibu lake.

27 Hata hivyo, baadhi ya Masadukayo, ambao husema hakuna ufufuo,^g wakaja na kumuuliza:^h **28** "Mwalimu, Musa alituandikia, 'Ndugu ya mtu akifa na kumwacha mke, lakini hakuwa na mtoto, ndu-

20:17 *Tnn., "kichwa cha pembeni."
20:22 *Au "sawa." 20:24 *Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 20

a Zb 118:22
Isa 28:16
Mt 21:42, 44
Mk 12:10, 11
Mdo 4:11
1Pe 2:7

b Isa 8:14, 15

c Mt 21:45, 46
Mk 12:12

d Mt 22:15-22
Mk 12:13-17

e Ro 13:7
Tit 3:1
1Pe 2:13

f Mt 22:21
Mk 12:17

g Mdo 23:8

h Mt 22:23-28
Mk 12:18-23

Safu ya 2

a Mwa 38:7, 8
Kum 25:5, 6

b Mt 22:29, 30
Mk 12:24, 25

c Kut 3:2, 6
Mt 22:31-33
Mk 12:26, 27

d Mt 22:32

e Mt 22:41-46
Mk 12:35-37

gu yake anapaswa kumchukua mke huyo ili kumwinulia ndugu yake uzao.^a **29** Basi kulikuwa na ndugu saba. Wa kwanza alioa mwanamke lakini akafa bila mtoto. **30** Na wa pili **31** na wa tatu, wakamwoa mwanamke huyo. Vivyo hivyo wote saba; walikufa bila kupata watoto. **32** Mwishowe pia yule mwanamke akafa. **33** Kwa hiyo, katika ufufuo, atakuwa mke wa nani? Kwa maana wote saba walikuwa wamemwoa."

34 Yesu akawaambia: "Watototo wa mfumo huu wa mambo* huoa na kuolewa, **35** lakini wale waliohesabiwa kuwa wanastahili kuupata mfumo huo wa mambo na kufufuliwa kutoka kwa wafu hawoi wala kuolewa.^b **36** Kwa kweli, hawawezi kufa tena kamwe, kwa maana wao ni kama malaika, nao ni watoto wa Mungu kwa kuwa watoto wa ufufuo. **37** Lakini hata Musa alifunua kwamba wafu watafufuliwa, katika masimulizi kuhusu kichaka cha miiba, anapomwita Yehova* 'Mungu wa Abrahamu na Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo.'^c **38** Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai, kwa maana kwake,* wote wako hai."^d **39** Baadhi ya waandishi wakasema: "Mwalimu, umesema vema." **40** Kwa maana hawakuwa tena na ujasiri wa kumuuliza hata swali moja.

41 Naye akawaambia: "Kwa nini watu husema kwamba Kristo ni mwana wa Daudi?^e

20:34 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo." 20:37 *Angalia Nyongeza A5. 20:38 *Au "kwa maoni yake."

42 Kwa maana Daudi mwenyewe anasema katika kitabu cha Zaburi, 'Yehova* alimwambia Bwana wangu: "Keti kwenye mkono wangu wa kume **43** mpaka niwaweke maadui wako kuwa kiti cha miguu yako."^a **44** Basi, Daudi anamwita Bwana; kwa hiyo anawezaje kuwa mwanawe?"

45 Watu wote walipokuwa wakimsikiliza, akawaambia wanafunzi wake: **46** "Jihadharini na waandishi wanaopenda kutembea wakiwa wamevaa kanzu na wanaopenda kusalimiwa sokoni, na viti vya mbele* katika masinagogi na mahali penye heshima zaidi kwenye milo ya jioni,^b **47** na ambao humaliza nyumba* za wajane na kutoa sala ndefu ili waonekane.[#] Hao watapatata hukumu kali[^] zaidi."

21 Yesu alipotazama, aliwaona matajiri wakitumbukiza zawadi zao katika masanduku* ya hazina.^c **2** Ndipo akamwona mjane mmoja maskini akitumbukiza sarafu mbili ndogo zenye thamani ndogo sana,^{*d} **3** naye akasema: "Kwa kweli ninawaambia, mjane huyu maskini ametumbukiza zaidi ya wote.^e **4** Kwa maana wote hao walitumbukiza zawadi kutokana na ziada yao, lakini mwanamke huyu ingawa ni maskini* alitumbukiza riziki yake yote."^f

5 Baadaye, watu fulani walipokuwa wakisema jinsi he-

20:42 *Angalia Nyongeza A5. 20:46 *Au "vilivyo bora." 20:47 *Au "mali." #Au "kuwa kisingizio." ^Au "nzito." 21:1 *Au "makasha." 21:2 *Tnn., "lep-toni mbili." Angalia Nyongeza B14. 21:4 *Au, "mwenye uhitaji."

SURA YA 20

a Zb 110:1
Mdo 2:34, 35
b Mt 23:2, 6, 7
Mk 12:38-40

SURA YA 21

c Mk 12:41
d Mk 12:42
e Mk 12:43, 44
Zko 8:12
f Mt 22:37

Safu ya 2

a Mt 24:1, 2
Mk 13:1, 2
b Lu 19:44
c Mt 24:3
Mk 13:4

d 2Ti 3:13
1Yo 4:1
Ufu 12:9

e Mt 24:4, 5
Mk 13:5, 6

f Mt 24:6
Mk 13:7

g Ufu 6:4

h Mt 24:7
Mk 13:8

i Mdo 11:28
Ufu 6:8

j Yoh 16:2

k Mt 10:17, 18
Mt 24:9
Mk 13:9
Mdo 25:23
Ufu 2:10

l Lu 12:11, 12

kalu lilivyopambwa kwa mawe mazuri na vitu vilivyowe kwa wakfu,^a **6** akawaambia: "Vitu hivi mnavyoona, siku zitakuja ambapo hakuna jiwe litakaloachwa juu ya jiwe lingine bila kuangushwa chini."^b **7** Ndipo wakamuuliza: "Mwalimu, kwa kweli mambo haya yatatukia lini, na ni ishara gani itakayoonyesha kwamba mambo haya yanakaribia kutokea?"^c **8** Akasema: "Jihadharini msipotoshwe,^d kwa maana wengi watakuja kwa msingi wa jina langu, wakisema, 'Mimi ndiye,' na, 'Wakati unaofaa umekaribia.' Msiwafuate.^e **9** Pia, mtakaposikia kuhusu vita na machafuko* msiogope. Kwa maana lazima mambo hayo yatukie kwanza, lakini ule mwisho hautatokea mara moja."^f

10 Kisha akawaambia: "Taifa litapigana na taifa,^g na ufalme kupigana na ufalme.^h

11 Kutakuwa na matetemeko makubwa ya ardhi, na magonjwa na upungufu wa chakula katika sehemu mbalimbali,ⁱ pia kutakuwa na mambo yenye kuogopesha na ishara kubwa kutoka mbinguni.

12 "Lakini kabla ya mambo hayo yote kutokea, watu watawakamata ninyi na kuwatesa/^j na kuwakabidhi kwenye masinagogi na magereza. Mtapelekwa mbele ya wafalme na magavana kwa sababu ya jina langu.^k **13** Hivyo, mtapata nafasi ya kutoa ushahidi. **14** Kwa hiyo, azimieni mioyoni mwenu kwamba hamtafanya mazoezi mape-ma kuhusu jinsi mtakavyojitetea,^l **15** kwa maana ni-

21:9 *Au "misukosuko."

tawapa maneno na hekima, ambayo wapinzani wenu wote kwa pamoja hawataweza ku-shindana nayo wala kubisha.^a **16** Zaidi ya hayo, mtakabidhiwa* hata na wazazi, ndugu, watu wa ukoo, na rafiki zenu, nao watawaua baadhi yenu,^b **17** nanyi mtachukiwa na watu wote kwa sababu ya jina langu.^c **18** Lakini hakuna hata unywele mmoja wa vichwa vyenu utakaoangamia.^d **19** Mktivumilia, mtaukoahai wenu.*^e

20 "Hata hivyo, mtakapoo-na Yerusalemu limezingirwa na majeshi yaliyopiga kambi,^f jueni kwamba linakaribia kuharibiwa.^g **21** Ndipo wale walio Yudea waanze kukimbilia milimani,^h na wale walio Yerusalemu waondoke, nao wale walio mashambani wasiingie ndani yake, **22** kwa sababu hizi ni siku za kutekeleza haki,* ili mambo yote yaliyoandikwa yatimizwe. **23** Ole wao wanawake wenye mimba na wale wanaonyonyesha mtoto katika siku hizo!ⁱ Kwa maana kutakuwa na mateso mengi katika nchi na ghadhabu dhidi ya watu hawa. **24** Nao wataangamizwa kwa upanga na watapelekwa utekwani katika mataifa yote;^j na Yerusalemu litakanyagwakanayaga na mataifa,* mpaka nyakati zilizowekwa za mataifa* zitimie.^k

25 "Pia, kutakuwa na ishara katika jua na mwezi na nyota,^l na duniani mataifa yatakuwa na maumivu makali bila

21:16 *Au "mtasalitiwa." 21:19 *Au "mtapata nafsi zenu." 21:22 *Au "siku za kisasi." 21:24 *Au "Watu wa mataifa."

SURA YA 21

a Mk 13:11
Mdo 6:8, 10

b Mik 7:6
Mk 13:12, 13
Mdo 7:59

c Mt 10:22
Mt 24:9

d Mt 10:29, 30
Lu 12:6, 7

e Mt 24:13
Ro 5:3, 4
Ebr 10:36
2Pe 1:5, 6

f Lu 19:43

g Da 9:26
Mt 23:37, 38
Mt 24:15, 16

h Mk 13:14

i Mt 24:19
Mk 13:17
Lu 23:28, 29

j Kum 28:64
Da 9:26

k Da 4:25

l Mt 24:29
Mk 13:24, 25

Safu ya 2

a Da 7:13

b Mt 24:30
Mk 13:26
Ufu 1:7

c Mt 24:32, 33
Mk 13:28, 29

d Mt 24:34
Mk 13:30

e Mt 24:35
Mk 13:31

f Isa 5:11, 12
Ro 13:13

g Met 11:4
Mt 6:25
1Ti 6:8

h 1Th 5:2, 3
2Pe 3:10

i Mt 25:13
Mk 13:33
1Ko 16:13
1Pe 5:8

j Ro 12:12
Efe 6:18
1Pe 4:7

k Mt 24:42
Mk 13:35
Ufu 6:16, 17
Ufu 16:15

kujuu cha kufanya kwa sababu ya mngurumo na msukosuko wa bahari. **26** Watu watazimia kwa woga wakitarajia mambo yatakayotokea juu ya dunia inayokaliwa, kwa maana nguvu za mbingu zitatikiswa. **27** Ndipo watakapomwona Mwana wa binadamu^a akija katika mawingu akiwa na nguvu na utukufu mwingi.^b **28** Lakini mambo hayo yatakapoanza kutukia, simameni wima na kuinua vichwa vyenu, kwa sababu ukombozi wenu unakaribia."

29 Ndipo akawaambia mfanono huu: "Angalieni mtini na miti mingine yote.^c **30** Inapochipua, mnaona na kujua kwamba kianguzi kinakaribia. **31** Vivyo hivyo, ninyi pia mtakapoo-na mambo hayo yakitukia, jueni kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia. **32** Kwa kweli ninawaambia, kizazi hiki hakitapitilia mbali kamwe mpaka mambo yote yatukie.^d **33** Mbingu na dunia zitapitilia mbali, lakini maneno yangu hayatapitilia mbali kamwe.^e

34 "Lakini jianganieni wenyewe ili mioyo yenu isileme-we kamwe na kula na kunywa kupita kiasif^f na mahangaiko ya maisha,^g na siku ile iwakute ghafla **35** kama mtego.^h Kwa maana itakuja juu ya wale wote wanaoishi juu ya uso wa dunia. **36** Basi, endeleeni kukeshaⁱ sikuzote mkiomba dua^j ili mfanikiwe kuponyoka mambo yote hayo ambayo lazima yatukie, na kusimama mbele ya Mwana wa binadamu."^k

37 Yesu alikuwa akifundi-sha hekaluni mchana, lakini

usiku alienda kukaa kwenye Mlima wa Mizeituni. **38** Watu wote walikuwa wakija hekalu-ni asubuhi na mapema ili wamsikilize.

22 Sasa Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu, inayoitwa, Pasaka,^a ilikuwa imekaribia.^b **2** Nao wakuu wa makuhani na waandishi walikuwa wakitafuta njia bora ya kumuua,^c kwa sababu waliwaogopa watu.^d **3** Ndi-po Shetani akamwingia Yuda, aliyetiwa Iskariote, ambaye alikuwa mmoja wa wale 12.^e **4** naye akaenda kuongea na wakuu wa makuhani na makapteni wa hekalu kuhusu jinsi atakavyomsaliti kwao.^f **5** Wakafurahisha na jambo hilo, nao wakakubaliana kumpa fedha.^g **6** Basi akakubali na kuanza kutafuta nafasi nzuri ya kumsaliti kwao bila umati kuwapo.

7 Siku ya Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu ikafika, siku ambayo dhabihu ya Pasaka hutolewa;^h **8** basi Yesu akawatuma Petro na Yohana, akawaambia: “Nendeni mkatutayarishie Pasaka tule.”ⁱ **9** Wakamuuliza: “Unataka tui-tayarishie wapi?” **10** Akawaambia: “Tazameni! Mtakapoi-ngia jijini, mtakutana na mwanamume akiwa amebeba mtungi wa maji. Mfuateni mwingie katika nyumba atakayoingia.” **11** Mwambieni mwenye nyumba hiyo, ‘Mwalimu anasema: “Kiko wapi chumba cha wage-ni ambamo ninaweza kula Pasaka pamoja na wanafunzi wangu?”’ **12** Mtu huyo atawaonyesha chumba kikubwa cha juu chenye vifaa. Tayarisheni humo.” **13** Basi wakaenda

SURA YA 22

a Law 23:5-8
Lu 22:7
Yoh 13:1

b Kut 12:3, 6

c Lu 9:22

d Mt 21:45, 46
Mt 26:3-5
Mk 14:1, 2
Lu 20:19

e Mt 26:14-16
Mk 14:10, 11
Yoh 6:70
Yoh 13:2, 27
Mdo 1:16, 17

f Yoh 13:18

g Zek 11:12

h Kut 12:14, 18
Kum 16:1, 2
Mt 26:17
Mk 14:12

i Kut 12:8

j Mt 26:18, 19
Mk 14:13-16

Safu ya 2

a Mt 26:20
Mk 14:17

b Kut 12:8

c 1Ko 10:16

d Ebr 10:10
1Pe 2:24

e Mt 26:27, 28
Mk 14:23, 24
1Ko 11:23-25

f Yer 31:31
Ebr 7:22
Ebr 8:8

g Kut 24:8

h Ebr 9:13, 14
1Pe 1:18, 19

i Zb 41:9
Mt 26:21
Mk 14:18
Yoh 13:21

j Isa 53:7, 8
Da 9:26
Mdo 4:27, 28

k Mt 26:24

l Mt 26:22
Mk 14:19
Yoh 13:22

m Mk 9:34
Lu 9:46

na kupata kama alivyokuwa amewaambia, nao wakaandaa Pasaka.

14 Wakati ulipofika, akake-ti mezani pamoja na mitume.^a **15** Akawaambia: “Nimetamani sana kula Pasaka hii pamoja nanyi kabla sijateseka; **16** kwa maana ninawaambia, sitakula tena Pasaka mpaka itakapotimizwa katika Ufalme wa Mungu.” **17** Yesu akapokea kikombe, akashukuru na kusema: “Chukueni kikombe hiki na mkipitishie kutoka kwa mmoja mpaka kwa mwingine kati yenu, **18** kwa maana ninawaambia, kuanzia sasa sitakunywa tena divai ya mzabibu mpaka Ufalme wa Mungu utakapokuja.”

19 Pia, akachukua mkate,^b akashukuru na kuumega, akawapa akisema: “Huu unamaanisha mwili wangu,^c ambao utatolewa kwa ajili yenu.^d Endeeleni kufanya hivi kwa kunikumbuka.”^e **20** Pia, akafanya vivyo hivyo na kile kikombe baada ya wao kula mlo wa jioni, akisema: “Kikombe hiki kinamaanisha agano jipya^f kwa msingi wa damu yangu,^g ambayo itamwagwa kwa ajili yenu.^h

21 “Lakini tazameni! mko-no wa msaliti wangu uko pamoja nami mezani.ⁱ **22** Kwa kweli, Mwana wa binadamu anenda zake kama ilivyotabiri-wa; lakini ole wake mtu atakayemsaliti!”^k **23** Kwa hiyo wakaanza kuulizana ni nani kati yao ambaye angemsaliti.^l

24 Hata hivyo, pia kukatokea bishano kali kuhusu ni nani aliyekuwa mkuu zaidi kati yao.^m **25** Lakini akawaambia: “Wafalme wa matai-

fa hupiga ubwana juu yao, na wale walio na mamlaka juu yao huitwa Wafadhili.^a **26** Hata hivyo, ninyi hampaswi kuwa hivyo.^b Lakini yule aliye mkuu zaidi kati yenu anapaswa kuwa mdogo zaidi,^c na yule anayehudumu. **27** Kwa maana ni nani aliye mkuu zaidi, yule anayekula* au yule anayehudumu?# Ni yule anayekula,* sivyo? Lakini mimi ni kama mtu anayehudumu# kati yenu.^d

28 "Hata hivyo, ninyi ndio mmeshikamana nami^e katika majaribu yangu;^f **29** nami ninafanya agano pamoja nanyi, kama Baba yangu alivyofanya agano pamoja nami, kwa ajili ya ufalme,^g **30** ili mle na kunywa mezani pangu katika Ufalme wangu,^h na kukeki kwenye viti vya ufalmeⁱ ili kuyahukumu makabila 12 ya Israeli.^j

31 "Simoni, Simoni, tazama! Shetani anataka kuwapata ninyi nyote ili awapepete kama ngano.^k **32** Lakini nimeomba dua kwa ajili yako ili imani yako isidhoofike;^l nawe utakaporudi, watie nguvu ndugu zako."^m **33** Petro akasema: "Bwana, niko tayari kwenda nawe gerezani na hata kufa nawe."ⁿ **34** Lakini akamwambia: "Petro ninakwambia, leo kabla jogoo hajawika utanikana mara tatu."^o

35 Akawauliza: "Nilipowatumama bila mkoba wa pesa, mfuko wa chakula, na viatu,^p je, mlikosa chochote?" Wakajibu: "Hapana!" **36** Kisha akawaambia: "Lakini sasa yule aliye na mkoba wa pesa au

22:27 *Au "anayeketi mezani." # Au "mtumishi."

SURA YA 22

a Mt 20:25-27
Mk 10:42-44
b 1Pe 5:2, 3
c Lu 9:46-48
d Mt 20:28
Yoh 13:3-5
Flp 2:5-7
e Yoh 6:67, 68
f Ebr 4:15
g Da 7:27
Lu 12:32
2Ti 2:12
Ebr 12:28
Yak 2:5
Ufu 1:6
h Lu 13:29
Yoh 17:24
i 1Ko 6:2
Ufu 2:26, 27
Ufu 3:21
Ufu 20:6
j Mt 19:28
k Mt 26:31
Mk 14:27
1Pe 5:8
l Yoh 17:15
m Ebr 12:12
n Mt 26:33
Mk 14:29
Yoh 13:37
o Mt 26:34
Mk 14:30
Lu 22:61
Yoh 13:38
p Mt 10:9, 10
Mk 6:7-9
Lu 9:2, 3

Safu ya 2

a Isa 53:12
b Lu 18:31
c Mt 26:30
Mk 14:26
Yoh 18:1
d Mt 26:41
Mk 14:38
Lu 22:46
e Mt 6:10
Mt 26:39
Mk 14:36
Yoh 5:30
Yoh 6:38
f 1Fa 19:5, 7
Da 10:18, 19
Mt 4:11
g Yoh 12:27
Ebr 5:7
h Mt 26:40
Mk 14:37
i Mt 26:41
Mk 14:38
Lu 22:40
j Mt 26:47-50
Mk 14:43-46
Yoh 18:2, 3

mfuko wa chakula aubebe, na yule asiye na upanga, auze vazi lake la nje anunue upanga. **37** Kwa maana ninawaambia mambo yaliyoandikwa kunihusu yatatimia, yaini, 'Naye alihesabiwa pamoja na waasi sheria.'^a Kwa maana hilo linatimia kunihusu."^b **38** Kisha wakasema: "Bwana, tazama! hapa pana panga mbili." Akawaambia: "Inatosha."

39 Alipoondoka, kama kawaida yake alienda kwenye Mlima wa Mizeituni, nao wanafunzi pia wakamfuata.^c **40** Walipofika huko akawaambia: "Endeleeni kusali ili msiingie katika majaribu."^d **41** Akawaacha na kwenda umbali wa mtupo wa jiwe, akapiga magoti na kuanza kusali, **42** akisema: "Baba, ukipenda, niondolee kikombe hiki. Hata hivyo, si kama ninavyopenda, bali mapenzi yako na yatendeke."^e **43** Ndipo malaika kutoka mbinguni akaja na kumtia nguvu.^f **44** Lakini alikuwa na maumivu makali hivi kwamba akaendelea kusali kwa bidii zaidi;^g na jasho lake likawa kama matone ya damu yakidondoka chini. **45** Baada ya kusali, akawaendea wanafunzi, akawakuta wakiwa wamelala usingizi, wakiwa wamechoka kwa sababu ya huzuni.^h **46** Akawaambia: "Kwa nini mnalala? Amkeni mwendelee kusali, ili msiingie katika majaribu."ⁱ

47 Alipokuwa bado akizungumza, tazama! umati ukaja ukiongozwa na Yuda, mmoja wa wale 12, naye akamkaribia Yesu ili ambusu.^j **48** Lakini Yesu akamuuliza: "Yuda,

unamsaliti Mwana wa binadamu kwa busu?" **49** Wale waliomzunguka walipoona jambo lililokuwa karibu kutukia, wakasema: "Bwana, tuwashambulie kwa upanga?" **50** Mmoja wao hata akampiga mtumwa wa kuhani mkuu na kumkata sikio la kulia.^a **51** Lakini Yesu akasema: "Inatosha." Akaligusa sikio la yule mtumwa akamponya. **52** Kisha Yesu akawauliza wakuu wa makuhani na makapteni wa hekalu na wazee waliokuja kumkamata: "Je, mme-kuja kunikamata mkiwa na mapanga na marungu kana kwamba mimi ni mwizi?"^b **53** Nilipokuwa pamoja nanyi hekaluni siku baada ya siku,^c hamkunikamata.^d Lakini huu ndio wakati wenu na mamlaka ya giza."^e

54 Ndipo wakamkamata,^f na kumpeleka nyumbani kwa kuhani mkuu; lakini Petro alikuwa akiwafuata kwa mbali.^g **55** Walipowasha moto kati-kati ya ua na kuketi chini pamoja, Petro alikuwa ameketi miongoni mwao.^h **56** Lakini kijakazi mmoja akamwona Petro akiwa ameketi kando ya moto, akamtazama kwa makini na kusema: "Mtu huyu pia alikuwa pamoja naye." **57** Lakini Petro akakana, akisema: "Wewe mwanamke, mimi simjui." **58** Baadaye kidogo mtu mwingine akamwona na kusema: "Wewe pia ni mmoja wao." Lakini Petro akasema: "Mimi si mmoja wao."ⁱ **59** Baada ya saa moja hivi kupita mwanamume mwingine akaanza kusisitiza kwa nguvu: "Kwa hakika mtu huyu pia alikuwa pamoja naye,

SURA YA 22

a Mt 26:51, 52
Mk 14:47
Yoh 18:10, 11

b Mt 26:55, 56
Mk 14:48, 49

c Lu 19:47

d Yoh 7:30

e Yoh 19:11

f Isa 53:7
Mdo 8:32

g Mt 26:57, 58
Mk 14:53, 54
Yoh 18:15

h Mt 26:69-75
Mk 14:66-72
Yoh 18:18

i Yoh 18:25-27

Safu ya 2

a Mt 26:75
Mk 14:72

b Zb 22:7

c Isa 50:6
Isa 53:5
Mt 26:67, 68
Mk 14:65

d Zb 2:2
Mt 27:1
Mk 15:1
Mdo 4:26

e Mt 26:63
Mk 14:61

f Da 7:13

g Zb 110:1
Mt 26:64
Mk 14:62
Mdo 2:32, 33
Mdo 7:55
Ro 8:34
Kol 3:1
Ebr 1:3

h Mt 26:65
Mk 14:63

kwa maana, yeye ni Mgalilaya!" **60** Lakini Petro akasema: "Wewe mtu, mimi sielewi unachosema." Mara tu alipokuwa akisema, jogoo akawika. **61** Ndipo Bwana akageuka, akamtazama Petro moja kwa moja, naye Petro akakumbuka maneno ambayo Bwana alimwambia: "Kabla jogoo hajakawika leo, utanikana mara tatu."^a **62** Naye akaenda nje akalialia kwa uchungu.

63 Sasa wale wanaume waliokuwa wamemkamata Yesu wakaanza kumdhihaki^b na kumpiga;^c **64** na baada ya kumfunika uso wakawa wakisema: "Toa unabii! Ni nani aliye-kupiga?" **65** Nao wakasema mambo mengine mengi ya kumkufuru.

66 Kulipokuwa mchana, kikundi cha wazee wa watu, yaani, wakuu wa makuhani na waandishi, wakakusanyika pamoja,^d nao wakampeleka katika jumba lao la Sanhedrini, na kumwambia: **67** "Ikiwa wewe ndiye Kristo, tuambie."^e Lakini akasema: "Hata nikiwaambia, hamtaamini hata kidogo. **68** Isitoshе, ikiwa ningewauliza, hamngenijibu. **69** Hata hivyo, tangu sasa Mwana wa binadamu^f ataketi kwenye mko-no wa kuume wenye nguvu wa Mungu."^g **70** Ndipo wote wakasema: "Kwa hiyo, je, wewe ndiye Mwana wa Mungu?" Akawajibu: "Ninyi wenyewe mnasema kwamba mimi ndiye." **71** Wakasema: "Kwa nini tutafute ushahidi zaidi? Kwa maana sisi wenyewe tumesikia kutoka kinywani mwake."^h

23 Kisha umati huo wote ukasimama na kumpeleka Yesu kwa Pilato.^a **2** Ndi-po wakaanza kumshtaki,^b wakisema: “Tulimkuta mtu huyu akipindua taifa letu na kuwakataza watu wasimlipe Kaisari kodi,^c akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo mfalme.”^d **3** Sasa Pilato akamuuliza: “Je, wewe ndiye Mfalme wa Wayahudi?” Akamjibu: “Wewe mwenyewe unasema hivyo.”^e **4** Ndipo Pilato akawaambia wakuu wa makuhani na ule umati: “Sioni mtu huyu akiwa na kosa lolote.”^f **5** Lakini wakasisitiza wakisema: “Anawachochea watu kwa kufundisha katika Yudea yote, kuanzia Galilaya mpaka hapa.” **6** Pilato aliposikia hivyo akauliza ikiwa Yesu alikuwa Mgalilaya. **7** Baada ya kuhakikisha kwamba alitoka katika eneo lililotawaliwa na Herode, akaagiza apelekwe kwa Herode,^g ambaye pia siku hizo alikuwa Yerusalemu.

8 Herode alipomwona Yesu alifurahi sana. Kwa maana kwa muda mrefu alitaka kumwona Yesu kwa sababu alikuwa amesikia mengi kumhusu,^h na alitamani kumwona akifanya miujiza. **9** Basi akaanza kumuuliza maswali mengi, lakini Yesu hakumjibu.ⁱ **10** Hata hivyo, wakuu wa makuhani na waandishi wakaendelea kusimama na kumshtaki kwa ukali. **11** Ndipo Herode na wanajeshi wake wakamtendea kwa dharau,^j naye Herode akamdhihaki^k kwa kumvika vazi la kifahari na kuagiza arudishwe kwa Pilato. **12** Siku hiyo Herode na Pilato wakawa

SURA YA 23

a Mt 27:2
Mk 15:1
Yoh 18:28

b Zb 35:11

c Mk 12:17

d Yoh 18:36

e Mt 27:11

f Yoh 18:38
Ebr 7:26
1Pe 2:21, 22

g Lu 3:1

h Mt 14:1
Mk 6:14
Lu 9:7-9

i Isa 53:7

j Isa 53:3

k Zb 22:7

Safu ya 2

a Yoh 18:38

b Mt 27:26
Yoh 19:1c Mt 27:20, 21
Mk 15:11
Yoh 18:40d Mt 27:22-26
Mk 15:12-15
Yoh 19:12

e Yoh 19:6

f Yoh 19:15, 16

marafiki, kwa maana kabla ya hapo walikuwa maadui.

13 Ndipo Pilato akawaita wakuu wa makuhani, watawala, na watu, **14** akawaambia: “Mliniletea mtu huyu mkisema anachochea watu kuasi. Tazama! Nilimhoji mbele yenu lakini sikupata msingi wa mashtaka yenu dhidi yake.”^a **15** Kwa kweli, hata Herode hakupata, ndiyo maana alimrudisha kwetu, tazama! ni wazi hajafanya jambo lolote linalostahili kifo. **16** Kwa hiyo nitamwadhibu^b na kumfungua.” **17** *— **18** Lakini umati wote ukasema kwa sauti kubwa: “Muue mtu huyu,* na utufungulie Baraba!”^c **19** (Mtu huyo alikuwa amefungwa gerezani kwa sababu ya mauaji na uchochezi uliokuwa umetokea jijini.) **20** Pilato akawapazia sauti tena, kwa sababu alitaka kumfungua Yesu.^d **21** Ndipo wakaanza kupiga kelele, wakisema: “Atundikwe mtini! Atundikwe mtini!”^e **22** Akawaambia mara ya tatu: “Kwa nini? Amefanya kosa gani? Mimi sikuona jambo lolote linalofanya astahili kifo; kwa hiyo nitamwadhibu kisha nimfungue.” **23** Lakini wakazidi kusesitiza, wakidai kwa sauti kubwa, kwamba auawe,* na sauti zao zikashinda.^f **24** Basi Pilato akaamua kutimiza dai lao. **25** Akamfungua yule mtu waliyemtaka, ambaye alikuwa amefungwa gerezani kwa sababu ya uchochezi na mauaji, lakini akamkabidhi Yesu

23:17 *Angalia Nyongeza A3. 23:18 *Tnn., “Mwondoe mtu huyu.” 23:21 *Au “Auawe kwenye mti! Auawe kwenye mti!” 23:23 *Au “auawe kwenye mti.”

mikononi mwao ili wamtendee wanavyopenda.

26 Walipokuwa wakienda naye, wakamshika Simoni wa Kirene, aliyekuwa akitoka mashambani, nao wakamtwika mti wa mateso* aubebe na kumfuata Yesu.^a **27** Watu wengi walikuwa wakimfuata, kutia ndani wanawake waliokuwa wakijipigapiga kwa huzuni na kumwombolezea. **28** Yesu akawageukia wanawake hao na kuwambia: “Binti za Yerusalemu, acheni kunililia. Bali jililieni ninyi wenyewe na watoto wenu;^b **29** kwa maana tazama! siku zinakuja ambapo watu watasema, ‘Wenye furaha ni wanawake walio tasa, wanawake ambao hawakuzaa, na wanawake ambao hawakunyonyesha!’^c **30** Ndiyo wataanza kuiambia milima, ‘Tu funkeni!’^d **31** Ikiwa wanafanya mambo haya wakati mti ni mbichi, itakuwaje utakapokauka?”

32 Wanaume wengine wawili, wahalifu, walikuwa pia wakipelekwa wakauawe pamoja naye.^e **33** Walipofika mahali panapoitwa Fuvu la Kichwa,^f wakamtundika Yesu kwenye mti pamoja na wale wahalifu, mmoja upande wake wa kume na mwingine upande wake wa kushoto.^g **34** Lakini Yesu alikuwa akisema: “Baba, wasamehe, kwa maana hawajui wanachofanya.” Isitoshe, wakapiga kura ili wagawane mavazi yake.^h **35** Watu walikuwa wamesimama hapo wakitazama. Lakini wale viongozi walikuwa wakimdhihakiki na kusema: “Aliwaokoa wengine;

SURA YA 23

a Mk 15:21
Yoh 19:17

b Mk 13:17

c Mt 24:19
Lu 21:23

d Ho 10:8

e Isa 53:12
Mt 27:38

f Mt 27:33

g Yoh 19:17, 18

h Zb 22:18
Mt 27:35
Mk 15:24
Yoh 19:24

Safu ya 2

a Zb 22:7, 8
Mt 27:42, 43
Mk 15:31

b Zb 69:21

c Mt 27:37
Mk 15:26
Yoh 19:19

d Mt 27:44
Mk 15:32

e Lu 1:32, 33

f Isa 11:6
Isa 35:1
Isa 65:17
Mdo 24:15
Ufu 21:1

g Mt 27:45
Mk 15:33

h Kut 26:31-33

i Ebr 10:19, 20

j Zb 31:5

k Mt 27:50

l Mt 27:54

mwacheni ajiokoe mwenyewe, ikiwa yeye ndiye Yule Aliyechaguliwa, Kristo wa Mungu.”^a **36** Hata wale wanajeshi wakamdhihaki, wakamkaribia na kumpa divai kali^b **37** wakisema: “Ikiwa wewe ndiye Mfalme wa Wayahudi, jiokoe.” **38** Kulikuwa pia na maandishi haya juu yake: “Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi.”^c

39 Ndiyo mmoja wa wale wahalifu waliotundikwa akaanza kumtukana^d akisema: “Wewe ndiye Kristo, sivyo? Jiokoe na utuokoe sisi pia!” **40** Yule mwingine akamkemea akisema: “Je, wewe humwogopi Mungu hata kidogo, kwa kuwa umepata hukumu ileile? **41** Sisi tunastahili kuteseka kwa sababu ya makosa tuliyoifanya; lakini mtu huyu hakufanya kosa lolote.”

42 Kisha akasema: “Yesu, unikumbuke utakapoingia katika Ufalme wako.”^e **43** Yesu akamwambia: “Kwa kweli ninakuambia leo, utakuwa pamoja nami katika Paradiso.”^f

44 Sasa, karibu saa sita,^{*} kukawa na giza katika nchi yote mpaka saa tisa,^g

45 kwa sababu hakukuwa na nuru ya jua; kisha pazia la patakatifu^h likapasuka katikati.ⁱ

46 Naye Yesu akapaza sauti na kusema: “Baba, naiweka roho yangu mikononi mwako.”^j Baada ya kusema hayo akafa.^{**k} **47** Alipoona mambo yaliyotokea, ofisa wa jeshi akaanza kumtukuzua Mungu, akisema: “Kwa kweli mtu huyu alikuwa mwadilifu.”^l **48** Na watu wote waliokuwa wamekusanyika hapo ili kuona tukio

23:44 *Yaani, karibu saa 6 mchana. #Yaani, karibu saa 9 alasiri. 23:46 *Au “akakata pumzi.”

hilo, walipoona mambo yaliyotukia, wakarudi nyumbani wakijipigapiga vifua. **49** Wale wote waliomfahamu walikuwa wamesimama mbali kidogo. Pia, wanawake waliokuwa wamefuatana naye kutoka Galilaya, walikuwa hapo na waliona mambo hayo.^a

50 Na tazama! kulikuwa na mwanamume aliyeitwa Yosefu, mshiriki wa Baraza, ambaye alikuwa mtu mwema na mwadilifu.^b **51** (Mtu huyo hakupiga kura kuunga mkono njama na kitendo chao.) Alikuwa wa kutoka Arimathea, jiji la Wayudea, naye alikuwa akiungojea Ufalme wa Mungu. **52** Mtu huyo alienda kwa Pilato akaomba apewe mwili wa Yesu. **53** Naye akaushusha^c na kuufunga kwa kitani bora, akaulaza katika kaburi* lili-lochungwa kwenye mwamba,^d ambamo hakuna mtu aliyewahi kulazwa. **54** Ilikuwa siku ya Matayarisho,^e na Sabato^f ilikuwa inakaribia kuanza. **55** Lakini wanawake waliokuja naye kutoka Galilaya, wa-kaenda kutazama kaburi* na jinsi mwili wake ulivyolazwa,^g **56** kisha wakarudi kutayarisha manukato na mafuta yenye marashi. Lakini, bila shaka, walipumzika siku ya Sabato^h kulingana na Sheria.

24 Hata hivyo, siku ya kwanza ya juma asubuhi na mapema, walienda kwenye kaburi,* wakiwa na manukato waliyotayarisha.ⁱ **2** Lakini wakakuta jiwe limeviringishwa kutoka kwenye kaburi,*^j **3** nao walipoingia, hawakuupata mwili wa Bwana Yesu.^k

23:53, 55; 24:1, 2, 12 *Au "kaburi la ukumbusho."

SURA YA 23

a Mt 27:55, 56
Mk 15:40, 41
Lu 8:2, 3

b Mt 27:57-60
Mk 15:43-46
Yoh 19:38

c Kum 21:22, 23

d Isa 53:9

e Mk 15:42
Yoh 19:42

f Kut 20:9, 10
Kum 5:13, 14

g Mt 27:61
Mk 15:47

h Kut 16:29
Kut 20:9, 10
Kut 31:15
Kum 5:12

SURA YA 24

i Mt 28:1
Mk 16:1, 2
Yoh 20:1

j Mt 28:2
Mk 16:4

k Mk 16:5

Safu ya 2

a Mt 28:5-7
Mk 16:5-7

b Yon 1:17
Mt 16:21
Mk 8:31
Lu 9:22

c Yoh 2:22

d Mt 28:8

4 Wakiwa wameshangazwa na jambo hilo, tazama! wanau-me wawili waliovaa mavazi yanayong'aa wakasimama kando yao. **5** Wanawake hao wakagogopa sana wakainamisha nyuso zao, basi wale wanaume wakawaambia: "Kwa nini mnamtafuta yule aliye hai kati ya wafu?"^a **6** Hayupo hapa, amefufuliwa. Kumbukeni jinsi alivyowaambia alipokuwa Galilaya, **7** kwamba Mwana wa binadamu lazima atiwe mikononi mwa wenye dhambi na kuuawa kwenye mti na siku ya tatu afufuliwe."^b **8** Ndipo wakakumbuka maneno yake,^c **9** wakarudi kutoka kaburini,* wakawaambia mambo hayo yote wale 11 na wengine wote.^d **10** Walikuwa Maria Magdalene, Yoana, na Maria mama ya Yakobo. Pia, wanawake wengine waliokuwa pamoja nao waliwaambia mitume mambo hayo. **11** Hata hivyo, waliyaona maneno hayo kama upuuzi, nao hawakuwaamini wanawake hao.

12 Lakini Petro akatoka, akakimbia hadi kwenye kaburi,* na alipoinama mbele, akaona vile vitambaa vya kitani peke yake. Kwa hiyo akaondoka akiwa ameshangazwa na mambo yaliyotokea.

13 Lakini tazama! siku hiyohiyo wanafunzi wawili walikuwa wakisafiri kwenda kijiji kinachoitwa Emau, kilicho karibu kilomita 11* kutoka Yerusalemu, **14** nao walikuwa wakizungumza kuhusu mambo hayo yote yaliyotukia.

24:9 *Au "kwenye kaburi la ukumbusho." 24:13 *Tnn., "stadia 60." Stadia moja ilikuwa sawa na mita 185 (futi 606.95). Angalia Nyongeza B14.

15 Sasa walipokuwa wakio-
ngea na kujadiliana kuhusu
mambo hayo, Yesu akakaribia
na kuanza kutembea pamoja
nao, 16 lakini macho yao yalizuiwa wasiweze
kumtambua.^a 17 Akawauliza:
“Ni mambo gani haya mna-
yojadiliana huku mkitembea?”
Nao wakasimama tuli, wakiwa
na huzuni. 18 Yule aliyelitwa
Kleopa akamjibu: “Je, wewe
ni mgeni anayekaa peke yake
Yerusalemu hivi kwamba hajui*
mambo ambayo yametukia huko
siku hizi?” 19 Akawauliza:
“Mambo gani?” Wakamjibu:
“Kuhusu Yesu Mnazareti,^b
yule nabii aliyefanya miujiza
na kusema maneno yenyewe
nguvu mbele za Mungu na watu
wote;^c 20 na jinsi wakuu wa
makuhani wetu na watawala
walivyomtoa ili ahukumiwe
kifo,^d kisha wakamtundika
kwenye mti. 21 Tulitazamia
kwamba yeye ndiye angekomboa
Israeli.^e Ndiyo, isitoshe hii ni
siku ya tatu tangu mambo hayo
yatokee. 22 Pia, wanawake
fulani miongoni mwetu walitushangaza,
kwa sababu walienda mapema
kwenye kaburi^{*f} 23 na walipokosa
kuuona mwili wake, wakarudi
wakisema pia waliona maono
yasiyo ya kawaida ya malaika
waliowaaambia kwamba Yesu
yuko hai. 24 Kisha baadhi ya
wenzetu wakaenda kwenye kaburi,
*g wakalikuta kama vile wale
wanawake walivyosema, lakini
hawakumwona.”

25 Basi akawaambia: “Enyi
wasio na akili na wagumu

24:18 * Au labda, “Je, wewe ni mgeni pekee katika Yerusalemu ambaye hajui?”
24:22, 24 * Au “kaburi la ukumbusho.”

SURA YA 24

a Yoh 20:14
Yoh 21:4

b Mt 2:23
Mt 21:11

c Kum 18:18
Lu 7:15, 16
Yoh 3:2
Yoh 6:14
Mdo 2:22

d Lu 23:1
Mdo 3:13
Mdo 13:27, 28

e Mdo 1:6

f Mt 28:1, 8
Lu 24:9-11

g Lu 24:12
Yoh 20:3

Safu ya 2

a Zb 22:16-18
Isa 53:7-9
1Ko 15:3

b Flp 2:9-11
Ebr 2:9
1Pe 1:11

c Yoh 1:45
Mdo 10:43
Mdo 26:22

d Mt 14:19
Mt 15:36
Mk 6:41

e Yoh 20:19

f 1Ko 15:3, 5

g Lu 24:30, 31

h Yoh 20:21

kuamini mambo yote yaliyose-
mwa na manabii! 26 Je, hai-
kuwa lazima Kristo kupata-
wa na mateso haya^a kisha ai-
ngie kwenye utukufu wake?”^b
27 Naye akawafanulia kuan-
zia Musa na Manabii wote,^c
mambo yote ambayo Maandiko
yalisema kumhusu.

28 Mwishowe walipokaribia
kijiji walichokuwa wakienda,
Yesu akajifanya kana kwamba
anaendelea na safari. 29 La-
kini wakamsihi asiende, waki-
sema: “Kaa pamoja nasi, kwa
sababu ni jioni, na siku ina-
karibia kwisha.” Basi akaingia
ili akae pamoja nao. 30 Naye
alipokuwa akila* pamoja nao
akauchukua mkate, akaubari-
ki, akaumeza na kuanza ku-
wapa.^d 31 Ndipo macho yao
yakafunguliwa kikamili nao
wakamtambua; lakini akato-
weka.^e 32 Wakaambiana:
“Je, mioyo yetu haikuwa iki-
waka alipokuwa akizungu-
mza nasi barabarani, na ali-
pokuwa akitufungulia* Maan-
diko waziwazi?” 33 Saa
hiyohiyo wakaondoka na ku-
rudi Yerusalemu, wakawakuta
wale 11 na watu waliokusanyi-
ka pamoja nao, 34 wakase-
ma: “Kwa kweli Bwana alifufu-
liwa naye alimtokea Simoni!”^f
35 Kisha wakasimulia mambo
yaliyotokea barabarani na ji-
nsi walivyomtambua alipou-
mega mkate.^g

36 Walipokuwa wakisema
mambo hayo Yesu akasi-
sama katikati yao na kuwa-
ambia: “Na muwe na amani.”^h

37 Lakini kwa sababu waliku-
wa wameshtuka na kuogopa,

24:30 * Au “alipokuwa ameketi mezani.”
24:32 * Au “akitufanulia.”

kuwa wameshtuka na kuogopa, walidhani kwamba wanao-na roho. **38** Basi akawauliza: “Kwa nini mnahangaika, na kwa nini mna shaka mioyoni mwenu? **39** Angalieni mikono na miguu yangu, kwamba ni mimi; niguseni mwone, kwa maana roho haina nyama na mifupa kama vile mnavyoona nilivyo.” **40** Alipokuwa akisema hayo, akawaonyesha mikono yake na miguu yake. **41** Wakiwa bado hawaamini kwa sababu ya shangwe nyingi na mshangao, akawauliza: “Mna chakula chochote hapa?” **42** Basi wakampa kipande cha samaki wa kuchomwa, **43** akakichukua, akala wakimtazama.

44 Kisha akawaambia: “Haya ndiyo maneno niliyowaambia nilipokuwa bado pamoja nanyi,^a kwamba mambo yote yaliyoandikwa kunihusu katika Sheria ya Musa, Manabii, na Zaburi lazima yatimizwe.”^b **45** Ndipo akafungua akili zao

SURA YA 24

a Mt 16:21
Lu 9:22

b Lu 24:27

Safu ya 2

a Yoh 12:16

b Isa 53:5
Mk 9:31

c Mdo 5:31

d Gal 3:14

e Mdo 4:1, 2
Mdo 5:27, 28f Yoh 15:26, 27
Mdo 1:8g Yoe 2:28
Yoh 14:16
Mdo 1:4, 5
Mdo 2:1, 4

h Mdo 1:9

i Yoh 16:22
Mdo 1:12

j Mdo 2:46, 47

ili waelewe kabisa maana ya Maandiko,^a **46** naye akawaambia: “Imeandikwa kwamba Kristo atateseka na kufufuliwa kutoka kwa wafu siku wa tatu,^b **47** na kwa msingi wa jina lake, toba kwa msamaha wa dhambi^c ingehubiriwa katika mataifa yote^d—kuanzia Yerusalemu.^e **48** Ninyi mtakuwa mashahidi wa mambo haya.^f **49** Na tazama! Nitawatumia kile ambacho Baba yangu ameahidi. Hata hivyo, kaeni jijini mpa-ka mtakapovikwa nguvu kutoka juu.”^g

50 Kisha akawaongoza mpa-ka Bethania, naye akainua mikono yake na kuwabariki. **51** Alipokuwa akiwabariki akatenganishwa nao, akaanza kuchukuliwa juu mbinguni.^h **52** Wakamsujudia* na kurudi Yerusalemu wakiwa na shangwe kubwa.ⁱ **53** Nao walikuwa hekaluni kila siku wakimsifu Mungu.^j

24:52 * Au “Wakamwinamia.”

KULINGANA NA

YOHANA

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Neno akawa mwili (1-18)
Ushahidi uliotolewa na Yohana Mbatizaji (19-28)
Yesu, Mwanakondoo wa Mungu (29-34)
Wanafunzi wa kwanza wa Yesu (35-42)
Filipo na Nathanaeli (43-51)</p> <p>2 Harusi huko Kana; abadili maji kuwa divai (1-12)
Yesu asafisha hekalu (13-22)
Yesu anajua kilicho ndani ya mwanadamu (23-25)</p> | <p>3 Yesu na Nikodemo (1-21)
Kuzaliwa tena (3-8)
Mungu aliupenda ulimwengu (16)
Yohana atoa ushahidi wa mwisho kumhusu Yesu (22-30)
Yule aliyetoka juu (31-36)</p> <p>4 Yesu na mwanamke Msamaria (1-38)
Mwabudu Mungu “kwa roho na kweli” (23, 24)
Wasamaria wengi wamwamini Yesu (39-42)</p> |
|--|--|

- Yesu amponya mwana wa ofisa (43-54)
- 5 Mwanamume mgonjwa aponywa Bethzatha (1-18)
Yesu apewa mamlaka na baba yake (19-24)
Wafu watasikia sauti ya Yesu (25-30)
Ushahidi kumhusu Yesu (31-47)
- 6 Yesu alisha wanaume 5,000 (1-15)
Yesu atembea juu ya maji (16-21)
Yesu ndiye "mkate wa uzima" (22-59)
Wengi wakwazwa na maneno ya Yesu (60-71)
- 7 Yesu akiwa kwenye Sherehe ya Vibanda (1-13)
Yesu afundisha kwenye sherehe (14-24)
Maoni mbalimbali kumhusu Yesu (25-52)
- 8 Baba hutoa ushahidi kumhusu Yesu (12-30)
Yesu ndiye "nuru ya ulimwengu" (12)
Watoto wa Abrahamu (31-41)
"Kweli itawaweka ninyi huru" (32)
Watoto wa Ibilisi (42-47)
Yesu na Abrahamu (48-59)
- 9 Yesu amponya mwanamume aliyezaliwa kipofu (1-12)
Mafarisayo wamuuliza maswali mwanamume aliyeponywa (13-34)
Upofu wa Mafarisayo (35-41)
- 10 Mchungaji na kondoo (1-21)
Yesu ndiye mchungaji mwema (11-15)
"Nina kondoo wengine" (16)
Wayahudi wakutana na Yesu kwenye Sherehe ya Wakfu (22-39)
Wayahudi wengi wakataa kuamini (24-26)
"Kondoo wangu husikiliza sauti yangu" (27)
Mwana yuko katika muungano na Baba (30, 38)
Watu wengi ng'ambo ya Yordani waamini (40-42)
- 11 Kifo cha Lazaro (1-16)
Yesu awafaraji Martha na Maria (17-37)
Yesu amfufua Lazaro (38-44)
Njama ya kumuua Yesu (45-57)
- 12 Maria ammininia Yesu mafuta miguuni (1-11)
Yesu aingia kwa kishindo (12-19)
- Yesu atabiri kifo chake (20-37)
Ukosefu wa imani wa Wayahudi watimiza unabii (38-43)
Yesu alikuja kuuokoa ulimwengu (44-50)
- 13 Yesu aosha miguu ya wanafunzi wake (1-20)
Yesu amtambulisha Yuda kuwa msaliti (21-30)
Amri mpya (31-35)
"Mkiwa na upendo miongoni mwenu" (35)
Yesu atabiri Petro atamkana (36-38)
- 14 Yesu ndiye njia pekee ya kumkaribia Mungu (1-14)
'Mimi ndiye njia, kweli, na uzima' (6)
Yesu awaahidi wanafunzi roho takatifu (15-31)
"Baba ni mkuu kuliko mimi" (28)
- 15 Mfano wa mzabibu wa kweli (1-10)
Amri ya kuonyesha upendo kama wa Kristo (11-17)
'Hakuna aliye na upendo mkuu kuliko huu' (13)
Ulimwengu unawachukia wanafunzi wa Yesu (18-27)
- 16 Wanafunzi wa Yesu wataabili kifo (1-4a)
Kazi ya roho takatifu (4b-16)
Huzuni ya wanafunzi itageuka kuwa shangwe (17-24)
Yesu aushinda ulimwengu (25-33)
- 17 Yesu asali mara ya mwisho akiwa na wanafunzi wake (1-26)
Uzima wa milele ndio huu, kumjua Mungu (3)
Wakristo si sehemu ya ulimwengu (14-16)
"Neno lako ni kweli" (17)
"Nimewajulisha jina lako" (26)
- 18 Yuda amsaliti Yesu (1-9)
Petro atumia upanga (10, 11)
Yesu apelekwa kwa Anasi (12-14)
Petro amkana Yesu mara ya kwanza (15-18)
Yesu mbele ya Anasi (19-24)
Petro amkana Yesu mara ya pili na ya tatu (25-27)
Yesu mbele ya Pilato (28-40)
"Ufalme wangu si sehemu ya ulimwengu huu" (36)

- 19 Yesu apigwa na kudhihakiwa (1-7)
Pilato amuiliza tena Yesu maswali (8-16a)
Yesu atundikwa kwenye mti huko Golgotha (16b-24)
Yesu amfanyia mama yake maandalizi (25-27)
Yesu afa (28-37)
Yesu azikwa (38-42)
- 20 Kaburi tupu (1-10)
Yesu amtokea Maria Magdalene (11-18)
Yesu awatokea wanafunzi wake (19-23)

- Tomasi awa na shaka lakini baadaye asadikishwa (24-29)
Kusudi la kitabu hiki cha kukunjwa (30, 31)
- 21 Yesu awatokea wanafunzi wake (1-14)
Petro amhakikishia Yesu kwamba anampenda (15-19)
“Lisha kondoo wangu wadogo” (17)
Wakati ujao wa mwanafunzi aliyependwa na Yesu (20-23)
Umalizio (24, 25)

1 Hapo mwanzo Neno alikuwako,^a naye Neno alikuwa pamoja na Mungu,^b na Neno alikuwa mungu.*^c **2** Mwanzoni yeye alikuwa pamoja na Mungu. **3** Vitu vyote vilikuja kuwako kupitia kwake,^d na bila yeye hakuna hata kitu kimoja kilichokuja kuwako.

Kile ambacho kimekuja kuwako **4** kupitia kwake kilikuwa uzima, na uzima ulikuwa nuru ya wanadamu.^e **5** Nuru inang'aa gizani,^f lakini giza halijaishinda.

6 Kuna mtu aliyetumwa akiwa mwakilishi wa Mungu; jina lake lilikuwa Yohana.^g **7** Mtu huyo alikuja akiwa shahidi, ili atoe ushahidi kuhusu nuru,^h ili watu wa namna zote waamini kupitia kwake. **8** Yeye hakuwa nuru hiyo,ⁱ bali alikuja kutoa ushahidi kuhusu nuru hiyo.

9 Nuru ya kweli inayowaangazia watu wa aina zote ilikuwa karibu kuja ulimwenguni.^j **10** Alikuwa ulimwenguni,^k nao ulimwengu ulikuja kuwako kupitia kwa-

1:1 *Au “alikuwa wa kimungu.”

SURA YA 1

- a Kol 1:15
Ufu 19:11, 13
b Met 8:22, 30
c Isa 9:6
Yoh 1:18
Flp 2:5, 6
d Yoh 1:10
e Yoh 8:12
f Yoh 3:19
g Mt 3:1
Lu 3:2
h Mt 3:11
i Yoh 1:19, 20
j Mt 4:16, 17
Yoh 3:19
Yoh 12:46
1Yo 2:8
k Yoh 1:14

Safu ya 2

- a Mwa 1:26
IKo 8:6
Kol 1:16
Ebr 1:2
b Ro 8:14, 16
ZKo 6:18
Efe 1:5
1Yo 3:1
c Gal 3:26
d Yoh 3:3
1Pe 1:23
1Yo 3:9
e Flp 2:7
1Ti 3:16
Ebr 2:14
f Yoh 3:16
1Yo 4:9
g Yoh 8:58

ke,^a lakini ulimwengu haukumjua. **11** Alikuwa nyumbani kwake mwenyewe, lakini watu wake mwenyewe hawakumkubali. **12** Hata hivyo, wale wote waliompokea, aliwapa mamlaka ya kuwa watoto wa Mungu,^b kwa sababu walikuwa na imani* katika jina lake.^c **13** Nao hawakuzaliwa kutokana na damu, wala mapenzi ya mwili au mapenzi ya mwanadamu, bali kutokana na Mungu.^d

14 Kwa hiyo Neno akawa mwili,^e akakaa kati yetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu ulio kama wa mwana mzaliwa pekee^f kutoka kwa baba; naye alikuwa amejaa kibali cha Mungu* na kweli. **15** (Yohana alitoa ushahidi kumhusu, ndiyo, alisema kwa sauti kubwa: “Huyu ndiye niliyesema kumhusu, ‘Yule anayekuja nyuma yangu amenitangulia, kwa maana alikuwapo kabla yangu.’”)^g **16** Kwa maana sote tulipokea kutokana na wingi alio nao,

1:12 *Au “walionyesha imani.” 1:14

*Au “alijaa fadhili zisizostahiliwa.”

hata fadhili zisizostahiliwa juu ya fadhili zisizostahiliwa. **17** Kwa sababu Sheria ilitolewa kupitia Musa,^a lakini fadhili zisizostahiliwa^b na kweli zilikuja kupitia Yesu Kristo.^c **18** Hakuna mwanadamu ambaye amemwona Mungu wakati wowote,^d mungu mzaliwa pekee^e aliye kando ya Baba,^{*f} ndiye ameeleza kumhusu.^g

19 Huu ndio ushahidi aliotoa Yohana, Wayahudi wali-powatuma makuhani na Walawi kutoka Yerusalemu wakamuulize: “Wewe ni nani?”^h

20 Naye akakiri na hakukana, akisema: “Mimi siye Kristo.”

21 Nao wakamuuliza: “Basi, wewe ni nani? Je, wewe ndiye Eliya?”ⁱ Akajibu: “Mimi siye.” “Je, wewe ndiye yule Nabii?”^j Akajibu: “Hapana!” **22** Kwa hiyo wakamwambia: “Wewe ni nani? Tuambie ili tupate jibu la kuwapa wale waliotutuma. Unasema nini juu yako mwenyewe?” **23** Akasema: “Mimi ni mtu anayepaza sauti nyikani, ‘Nyoosheni njia ya Yehova,’^{*k} kama alivyosema nabii Isaya.”^l

24 Sasa wale waliotumwa walitoka kwa Mafarisayo. **25** Basi wakamuuliza: “Kwa nini unabatiza ikiwa wewe si Kristo au Eliya au yule Nabii?” **26** Yohana akawajibu: “Mimi ninabatiza katika maji. Kuna mtu aliyesimama miongoni mwenu msiyemjua, **27** yule anayekuja nyuma yangu, ambaye sistahili kufungua kamba za viatu vyake.”^m

28 Mambo hayo yalifanyika huko Bethania ng’ambo ya Yo-

1:18 *Au “kifuani pa Baba.” Inamaanisha mahali pa heshima ya pekee au pendeleo.” 1:23 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 1

a Kut 31:18

b Ro 3:23, 24
Efe 1:5, 6c Yoh 8:31, 32
Yoh 14:6
Yoh 18:37d Kut 33:17, 20
Yoh 6:46

e Yoh 1:1

f Met 8:22, 30

g Mt 11:27

h Lu 3:15

i Mal 4:5

j Kum 18:15
Yoh 6:14, 15
Yoh 7:37, 40
Mdo 3:22

k Isa 40:3

l Mt 3:1, 3
Mk 1:3
Lu 1:67, 76
Lu 3:3, 4
Lu 7:27, 28

m Mt 3:11

Safu ya 2

a Mt 3:1, 6

b Mdo 8:32, 35
1Pe 1:18, 19
Ufu 5:6c Isa 53:7, 11
1Ko 15:3
Ebr 9:13, 14
1Pe 2:24
1Yo 3:5d Yoh 6:51
1Yo 2:1, 2
1Yo 4:14

e Yoh 1:15

f Mdo 19:4

g Mt 3:16
Mk 1:10
Lu 3:22

h Mt 3:16

i Mt 3:11
Mdo 1:5
Mdo 2:1, 4

j Mt 3:17

k Ufu 5:12

rdani, ambako Yohana alikuwa akibatiza watu.^a

29 Siku iliyofuata alimwona Yesu akimjia, naye akasema: “Ona, Mwanakondoo^b wa Mungu ambaye huondoa dhambi^c ya ulimwengu!^d **30** Huyu ndiye niliyesema kumhusu: ‘Nyuma yangu anakuja mwana-mume ambaye amenitangulia, kwa sababu alikuwapo kabla yangu.’^e **31** Hata mimi sikumjua, lakini nilikuja kubatiza katika maji ili afunuliwe kwa Israeli.”^f **32** Yohana pia alitoa ushahidi akisema: “Nilionga roho ikishuka kama njiva kutoka mbinguni, nayo ika-kaa juu yake.^g **33** Hata mimi sikumjua, bali Yule aliyenituma nikabatiza katika maji ali-niambia: ‘Yeyote ambaye utao-na roho ikishuka na kukaa juu yake,^h huyo ndiye anayebatiza kwa roho takatifu.’ⁱ **34** Mimi nimeona, nami nimetoa ushahidi kwamba huyo ndiye Mwana wa Mungu.”^j

35 Tena siku iliyofuata, Yohana alikuwa amesimama pamoja na wawili kati ya wanafunzi wake. **36** Alipomtazama Yesu akipita akasema: “Ona, Mwanakondoo^k wa Mungu!”

37 Wanafunzi hao wawili walipomsikia akisema hivyo, wakamfuata Yesu. **38** Ndipo Yesu akageuka na alipowao-na wakimfuata, akawauliza: “Mnatafuta nini?” Wakamwambia: “Rabi (neni ambalo linapotafsiriwa linamaanisha, “Mwalimu”), unakaa wapi?”

39 Akawaambia: “Njoooni, nanyi mtaona.” Basi wakaenda na kuona mahali alipokuwa akikaa, nao wakakaa pamoja naye siku hiyo; ilikuwa ka-

ribu saa kumi.* **40** Andrea,^a ndugu ya Simoni Petro alikuwa mmoja wa wale wawili waliosikia mambo aliyosema Yohana na kumfuata Yesu. **41** Kwanza alimpata Simoni ndugu yake na kumwambia: “Tumempata Masihi!”^b (neno ambalo linapotafsiriwa linaamaanisha, “Kristo”), **42** kisha akampeleka kwa Yesu. Yesu akamtazama na kumwambia: “Wewe ni Simoni^c mwana wa Yohana; utaitwa Kefa” (linalotafsiriwa kuwa, “Petro”).^d

43 Siku iliyofuata Yesu alitaka kwenda Galilaya. Basi akamkuta Filipo^e na kumwambia: “Njoo uwe mfuasi wangu.” **44** Filipo alitoka Bethsaida, jiji walilotoka Andrea na Petro. **45** Filipo akamkuta Nathanaeli^f na kumwambia: “Tumempata yule ambaye Musa, katika Sheria, na Manabii waliandika kumhusu: Yesu, mwana wa Yosefu,^g kutoka Nazareti.” **46** Lakini Nathanaeli akamuuliza: “Je, kitu chochote kizuri kinaweza kutoka Nazareti?” Filipo akamjibu: “Njoo uone.” **47** Yesu alipomwona Nathanaeli aki-ja, akasema hivi kumhusu: “Ona, Mwisraeli kwa hakika ambaye hamna udanganyifu ndani yake.”^h **48** Nathanaeli akamuuliza: “Umenijua-je?” Yesu akamjibu: “Nilikuona ulipokuwa chini ya mtini, kabla ya Filipo kukuita.” **49** Nathanaeli akamwambia: “Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu, wewe ni Mfalme wa Israeli.”ⁱ **50** Yesu akasema: “Je, unaamini kwa sababu nimekuambia nilikuona chini ya

1:39 *Yaani, karibu saa 10 jioni.

SURA YA 1

a Mt 4:18

b Da 9:25

c Mt 10:2
Mdo 15:14

d Mt 16:18

e Mt 10:2, 3

f Mt 10:2, 3
Lu 6:13, 14g Mt 1:16
Mt 13:55
Lu 2:4

h Yoh 2:24, 25

i Mt 27:11
Lu 1:31, 32
Yoh 12:13

Safu ya 2

a Mwa 28:10, 12
Zb 104:4
Da 7:13
Mt 4:11
Lu 22:43

SURA YA 2

b Mk 7:3

mtini? Utaona mambo maku-bwa kuliko haya.” **51** Kisha akamwambia: “Kwa kweli ninawaambia, mtaona mbingu imefunguliwa na malaika wa Mungu wakipanda na kushuka kwa Mwana wa binadamu.”^a

2 Basi siku ya tatu kulikuwa na karamu ya ndoa katika Kana ya Galilaya, na mama ya Yesu alikuwa huko. **2** Yesu na wanafunzi wake pia walikuwa wamealikwa kwenye karamu hiyo ya ndoa.

3 Divai ilipopungua mama ya Yesu akamwambia: “Hawana divai.” **4** Lakini Yesu akamjibu: “Mwanamke, jambo hilo linatuhusuje mimi na wewe?” Bado saa yangu haijafika.” **5** Mama yake akawaambia wahudumu: “Fanyeni lolote atakalowaambia.” **6** Kulikuwa na mitungi sita ya maji hapo kulingana na sheria za utakaso za Wayahudi,^b kila mmoja ulikuwa na uwezo wa kuchukua vipimo* viwili au vitatu vya maji. **7** Yesu akawaambia: “Ijaze ni mitungi hiyo maji.” Nao wakajiza pomoni. **8** Akawaambia: “Choteni kidogo na kumpelekea msimamizi wa karamu.” Basi wakampeleka. **9** Msimamizi wa karamu alipoonja maji yaliyokuwa yamegeuzwa kuwa divai, bila kujua divai ilitoka wapi (lakini wahudumu waliokuwa wamechota maji hayo walijua), akamwita bwana harusi **10** akamwambia: “Kila mtu hutoa divai

2:4 *Tnn., “Nina nini nawe, mwanamke?” Hii ni nahau au msemu unaonyesha kukataa jambo. Matumizi ya neno “mwanamke” hayaonyeshi ukosefu wa heshima. **2:6** *Yaelekea kipimo hicho kilikuwa bathi iliyokuwa sawa na lita 22. Angalia Nyongeza B14.

nzuri kwanza, kisha hutoa divai hafifu wakati ambapo watu wameingiwa na kileo. Lakini wewe umehifadhi divai nzuri mpaka sasa.” **11** Yesu alifanya muujiza huo wake wa kwanza katika Kana ya Galilaya, kwa hiyo akaonyesha utukufu wake,^a na wanafunzi wake wakamwamini.

12 Baada ya hayo, Yesu, mama yake, ndugu zake,^b na wanafunzi wake wakashuka kwenda Kapernaumu,^c lakini hawakukaa huko siku nyingi.

13 Pasaka^d ya Wayahudi ilikuwa imekaribia, basi Yesu akapanda kwenda Yerusalemu. **14** Alipoingia hekaluni akakuta watu wakiuza ng’ombe, kondoo, na njiwa,^e pia, wale waliobadili pesa walikuwa kwenye viti vyao. **15** Basi akatengeza mjeledi wa kamba na kuwafukuza hekaluni wote waliokuwa na kondoo na ng’ombe, akamwaga sarafu za wale waliobadili pesa na kupindua meza zao.^f **16** Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa: “Ondoeni vitu hivi hapa! Acheni kuifanya nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara!”^g **17** Wanafunzi wake wakakumbuka kwamba imeandikwa: “Bidii kwa ajili ya nyumba yako itanila.”^h

18 Kwa hiyo, Wayahudi wakamuuliza: “Utatuonyesha ishara gani,ⁱ kwa maana unafanya mambo haya?” **19** Yesu akawajibu: “Libomoeni hekalu hili, na kwa siku tatu nitalisimamisha.”^j **20** Kisha Wayahudi wakasema: “Hekalu hili lilijengwa kwa miaka 46, je, wewe utalisimamisha kwa

SURA YA 2

a Isa 9:1, 2
Yoh 1:14

b Mt 13:55
Mk 3:31
Lu 8:19
Mdo 1:14

c Mt 4:13
d Kut 12:14
Hes 28:16
Kum 16:1
Yoh 11:55

e Law 1:14

f Mt 21:12
Mk 11:15, 16
Lu 19:45

g Yer 7:11
Mt 21:13
Mk 11:17
Lu 19:46

h Zb 69:9

i Mt 12:38
Mt 16:1
Yoh 4:48
Yoh 6:30

j Mt 26:59-61
Mt 27:39, 40
Mk 14:57, 58

Safu ya 2

a Mt 16:21

b Lu 24:6-8

c Mt 9:3, 4
Mk 2:6-8
Yoh 1:47, 48
Yoh 6:64
Ufu 2:23

SURA YA 3

d Yoh 7:50, 51
Yoh 19:39

e Yoh 12:42

f Yoh 1:38

g Yoh 2:11

h Yoh 14:11
Mdo 2:22
Mdo 10:38

i Yoh 1:12, 13
iPe 1:3, 23
iYo 3:9

j iKo 15:50

k Mt 28:19
Mdo 8:36
Mdo 10:47

l Mt 3:11
Mdo 1:5
Mdo 10:45
Mdo 19:5, 6

siku tatu?” **21** Lakini alikuwa akizungumza kuhusu hekalu la mwili wake.^a **22** Hata hivyo, alipofufuliwa kutoka kwa wafu, wanafunzi wake wakakumbuka alikuwa akisema jambo hilo,^b nao wakaamini andiko na maneno ambayo Yesu alikuwa amesema.

23 Hata hivyo, alipokuwa Yerusalemu kwenye sherehe ya Pasaka, watu wengi wakamwamini, kwa sababu waliona miujiza aliyokuwa akifanya.

24 Lakini Yesu alijihadhari nao kwa sababu aliwajua wote **25** na hakuhitaji mtu yeyote atoe ushahidi kuhusu mwanadamu, kwa maana alijua kilicho ndani ya mwanadamu.^c

3 Kulikuwa na Farisayo aliyetitwa Nikodemo,^d mtawala wa Wayahudi. **2** Alienda kwa Yesu usiku^e na kumwambia: “Rabi,^f tunajua kwamba wewe ni mwalimu na umetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna anayeweza kufanya miujiza^g kama unayofanya isipokuwa Mungu awe pamoja naye.”^h **3** Yesu akamwambia: “Kwa kweli ninakuambia, mtu asipozaliwa tena,ⁱ hawezi kuuona Ufalme wa Mungu.”^j **4** Nikodemo akamuuliza: “Mtu akiwa mzee anawezaje kuzaliwa tena? Hawezi kuingia tumboni mwa mama yake mara ya pili na kuzaliwa, sivyo?” **5** Yesu akajibu: “Kwa kweli ninakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji^k na roho,^l hawezi kuingia katika Ufalme wa Mungu. **6** Kile ambacho kimezaliwa kwa mwili ni mwili, na kile ambacho kimezaliwa kwa roho ni roho. **7** Usi-

3:3 *Au labda, “asipozaliwa kutoka juu.”

2:16 *Au “soko.”

shangae kwa sababu nimekuambia: Lazima ninyi mzaliwe tena. **8** Upepo huvuma mahali unapotaka, nawe unasia kiu ukivuma, lakini hujui mahali unapotoka wala mahali unapoenda. Ndivyo alivyo kila mtu ambaye amezaliwa kwa roho.”^a

9 Nikodemo akamuuliza: “Mambo haya yanawezekana-je?” **10** Yesu akamjibu: “Je, wewe ni mwalimu wa Israeli na bado hujui mambo haya? **11** Kwa kweli ninakuambia, yale tunayojua tunayasema, na yale ambayo tumeyaona tunatoa ushahidi kuyahusu, lakini ninyi hampokei ushahidi tunaotoa. **12** Ikiwa nime-wambia mambo ya duniani na bado hamyaamini, mtawezaje kuamini nikiwambia mambo ya mbinguni? **13** Isitoshe, hakuna mtu aliyepanda kwenda mbinguni^b ila yule aliyeshuka kutoka mbinguni,^c yaani, Mwana wa binadamu. **14** Kama vile Musa alivyoinua nyoka nyikani,^d ndivyo Mwana wa binadamu atakavyoinuliwa,^e **15** ili kila mtu anayemwamini apate uzima wa milele.”^f

16 “Kwa maana, Mungu aliupenda ulimwengu sana hivi kwamba akamtoa Mwana wake mzaliwa pekee,^g ili kila mtu anayemwamini* asiangamizwe bali awe na uzima wa milele.^h **17** Kwa maana Mungu hakumtuma Mwana-we ulimwengu ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe kupitia kwake.ⁱ **18** Yeyote anayemwamini* hatahukumiwa.^j Yeyote amba-

3:16 *Au “anayeonyesha kwamba anamwamini.” 3:18 *Au “anayeonyesha imani.”

SURA YA 3

a Ro 8:14, 16

b Mdo 2:34

c Yoh 6:38
Yoh 8:23, 42

d Hes 21:8, 9

e Yoh 8:28
Gal 3:13f Yoh 3:36
Yoh 20:31g Ro 5:8
Ro 8:32
1Yo 4:9, 10
1Yo 4:19h Yoh 6:40
Yoh 20:31
Ro 6:23
ZTi 3:15
1Yo 5:13i Lu 19:10
Yoh 12:47
1Ko 15:22
2Ko 5:18, 19
1Ti 1:15
1Yo 2:1, 2
1Yo 4:14

j Yoh 5:24

Safu ya 2

a Mt 10:33
Ebr 10:29b Yoh 1:9
Yoh 8:12
Yoh 9:5
Yoh 12:46c Yoh 12:36, 46
1Yo 1:7

d Yoh 4:2

e Mk 1:10
Mdo 8:38

f Mt 3:1, 5, 6

g Mt 14:3
Lu 3:19, 20

h Yoh 1:33, 34

ye hamwamini amehukumiwa tayari, kwa sababu hana imani* katika jina la Mwana mzaliwa pekee wa Mungu.^a **19** Basi huu ndio msingi wa hukumu: kwamba nuru imekuja ulimwengu,^b lakini watu wamependa giza badala ya nuru, kwa maana matendo yao yalikuwa maovu. **20** Kwa maana yeyote ambaye huzoea kutenda mambo maovu huchukia nuru na haji kwenye nuru, ili matendo yake yasikaripiwe.* **21** Lakini yeyote ambaye hufanya yaliyo ya kweli huja kwenye nuru,^c ili matendo yake yafunuliwe kwamba yamefanywa kulingana na Mungu.”

22 Baada ya mambo haya, Yesu na wanafunzi wake wa-kaenda katika maeneo ya mashambani ya Yudea, naye akakaa pamoja nao huko kwa muda fulani, akiwabatiza watu.^d **23** Lakini Yohana pia alikuwa akibatiza huko Ainoni karibu na Salimu, kwa sababu kulikuwa na maji mengi huko,^e na watu walikuwa wakija na kubatizwa;^f **24** kwa maana bado Yohana hakuwa amefungwa gerezani.^g

25 Wanafunzi wa Yohana walibishana na Myahudi fulani kuhusu utakaso. **26** Kwa hiyo wakaja kwa Yohana na kumwambia: “Rabi, mtu aliye-kuwa pamoja nawe ng’ambo ya Yordani, ambaye ulitoa ushahidi kumhusu,^h anabatiza na watu wote wanaenda kwake.” **27** Yohana akawaambia: “Mtu hawezi kupokea kitu chochote isipokuwa awe amepewa kutoka mbinguni.

3:18 *Au “haonyeshi imani.” 3:20 *Au “yasifunuliwe.”

28 Ninyi wenyewe mlishuhudia kwamba nilisema, 'Mimi si Kristo,^a bali, nimetumwa nimitangulie.'^b **29** Yule aliye na bibi harusi ndiye bwana harusi.^c Hata hivyo, rafiki ya bwana harusi, anaposimama na kumsikia, anashangilia sana kwa sababu ya sauti ya bwana harusi. Kwa hiyo shangwe yangu imekamilishwa. **30** Huyu lazima aendelee kuongezeka, lakini mimi lazima niondelee kupungua."

31 Yule anayetoka juu^d yuko juu ya watu wote. Yule anayetoka duniani, ni wa kutoka duniani na husema kuhusu mambo ya duniani. Yule anayetoka mbinguni, yuko juu ya watu wote.^e **32** Yeye hutoa ushahidi kuhusu mambo aliyoota na kusikia,^f lakini hakuna mtu anayekubali ushahidi wake.^g **33** Yeyote ambaye amekubali ushahidi wake ametia muhuri wake* kwamba Mungu ni wa kweli.^h **34** Yule ambaye Mungu amemtuma husema maneno ya Mungu,ⁱ kwa maana Mungu hutoa roho yake kwa wingi.* **35** Baba anampenda Mwana/naye amekabidhi vitu vyote mkononi mwake.^k **36** Yule anayemwamini Mwana ana uzima ya milele;^l yule asiye mtii Mwana hataona uzima,^m bali ghadhabu ya Mungu hu-kaa juu yake.ⁿ

4 Bwana alipojua kwamba Mafarisayo walikuwa wamesikia kuwa Yesu alikuwa akifanya na kubatiza^o wanafunzi wengi kuliko Yohana— **2** ingawa Yesu hakubatiza bali wanafunzi wake

3:33 *Au "amethibitisha." **3:34** *Au "hatoi roho kwa kipimo."

SURA YA 3

a Yoh 1:19, 20

b Mt 11:7, 10
Lu 1:13, 17

c 2Ko 11:2
Efe 5:25
Ufu 21:9

d Yoh 8:23

e Mt 3:11

f Yoh 8:26
Yoh 15:15

g Yoh 1:11
Yoh 3:11

h 1Yo 5:10

i Yoh 7:16

j Yoh 5:20
Yoh 15:9, 10

k Mt 11:27
Lu 10:22

l Yoh 3:16
Yoh 6:47
Ro 1:17
Ebr 5:9

m 2Th 1:7, 8
1Yo 5:12

n Efe 5:5, 6
Ebr 10:26, 27

SURA YA 4

o Yoh 3:22

Safu ya 2

a Mwa 33:18, 19
Yos 24:32

b Yoh 4:12

c 2Fa 17:24
Mdo 10:28

d Efe 2:8

e Yoh 7:37

ndio waliokuwa wakibatiza— **3** akaondoka Yudea na kuelekea tena Galilaya. **4** Lakin alipaswa kupitia Samaria. **5** Basi akafika katika jiji moja la Samaria linaloitwa Sikari, lililokuwa karibu na shamba ambalo Yakobo alimpa Yosefu^a mwana wake. **6** Kisima cha Yakobo kilikuwa hapo.^b Basi Yesu, kwa kuwa alikuwa amechoka kwa sababu ya safari, akaketi kando ya kisima hicho.* Ilikuwa karibu saa sita.[#]

7 Mwanamke Msamaria akaja kuteka maji. Yesu akamwambia: "Naomba maji ninywe." **8** (Kwa maana wanafunzi wake walikuwa wameenda jijini kununua chakula.) **9** Kwa hiyo mwanamke huyo Msamaria akamuuliza: "Wewe ni Myahudi, nami ni mwanamke Msamaria, unawezaje kuniomba maji ya kunywa?" (Kwa maana Wayahudi hawashirikiani na Wasamaria.)^c **10** Yesu akamjibu: "Kama ungejua zawadi ya bure inayotoka kwa Mungu^d na ni nani ambaye anakumbia, 'Naomba maji ninywe,' ungemwamba, naye angekupa maji yaliyo hai."^e **11** Akamwambia: "Bwana, huna hata ndoo ya kutekea maji, na kisima ni kirefu. Basi, umeyatoa wapi hayo maji yaliyo hai? **12** Je, wewe ni mkuu kuliko babu yetu Yakobo, aliyetupatia kisima hiki ambacho yeye pamoja na wanawe na mifugo yake walikunywa maji yake?" **13** Yesu akamjibu: "Kila mtu anayekunywa maji haya ata-

4:6 *Au "chemchemi hiyo; au mabubujiko hayo." [#]Yaani, karibu saa 6 mchana.

kuwa na kiu tena. **14** Yeyote atakayekunywa maji nitakayompa hatakuwa na kiu kamwe,^a kwa sababu maji ambayo nitampa yatakuwa kama chemchemi ya maji ndani yake, inayobubujika ili kumpa uzima wa milele.”^b **15** Yule mwanamke akamwambia: “Bwana, nipe maji hayo ili nisiwe na kiu tena wala nisiendelee kuja hapa kuteka maji.”

16 Yesu akamwambia: “Nenda ukamwite mume wako uje naye hapa.” **17** Mwanamke huyo akajibu: “Sina mume.” Yesu akamwambia: “Umesema kweli kwamba huna mume. **18** Kwa maana ume kuwa na waume watano, na mwanamume uliye naye sasa si mume wako. Hapo umesema kweli.” **19** Yule mwanamke akamwambia: “Bwana, ninaona kwamba wewe ni nabii.”^c **20** Mababu zetu waliabudu katika mlima huu, lakini ninyi mnasema tunapaswa kumwabudu Mungu huko Yerusalemu.”^d **21** Yesu akamwambia: “Mwanamke, niamini, saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu wala kule Yerusalemu. **22** Ninyi mnaabudu msichokijua;^e sisi tunaabudu tuna chokijua, kwa sababu wokovu huanza kwa Wayahudi.”^f **23** Hata hivyo, saa inakuja, nayo ipo sasa, ambayo waabudu wa kweli watamwabudu Baba kwa roho na kweli, kwa maana kwa kweli, Baba anatafuta watu wa namna hiyo wamwabudu.^g **24** Mungu ni Roho,^h na wale wanaomwabudu lazima wamwabudu kwa roho na kweli.”ⁱ **25** Huyu mwanamke akamwambia: “Ni-

SURA YA 4

a Yoh 6:35

b Yoh 7:38
Ro 6:23
1Yo 5:20c Lu 7:16
Yoh 9:17d Kum 12:5, 6
1Fa 9:3
2Nya 7:12
Zb 122

e 2Fa 17:29, 33

f Isa 2:3
Ro 9:4

g 2Nya 16:9

h 2Ko 3:17
1Ti 1:17
Ebr 11:27

i Ro 12:1

Safu ya 2

a Yoh 9:35-37

b Yoh 1:38

c Yoh 6:38

d Yoh 5:30, 36
Yoh 17:4
Yoh 19:30

e Mt 9:37

f 1Ko 3:8

najua kwamba Masihi anakujaja, anayeitwa Kristo. Atakapokuja, atatutangazia mambo yote waziwazi.” **26** Yesu akamwambia: “Mimi ninayezungumza nawe, ndiye.”^a

27 Ndipo wanafunzi wake wakaja, wakashangaa kwa sababu alikuwa akiongea na mwanamke. Hata hivyo, haku na yeyote aliyemuuliza: “Unatafuta nini?” au, “Kwa nini unaongea naye?” **28** Basi, yule mwanamke akauacha mtungi wake wa maji akaenda jijini na kuwaambia watu: **29** “Twendeni mkamwone mtu aliyeniambia kila kitu nilichofanya. Je, inawezekana kwamba yeye ndiye Kristo?” **30** Wakatoka jijini wakaenda kumwona Yesu.

31 Wakati huohuo wanafunzi walikuwa wakimhimiza: “Rabi,^b kula.” **32** Lakini akawaambia: “Nina chakula ambacho hamkijui.” **33** Kwa hiyo wanafunzi wakaambiana: “Hakuna mtu aliyemletea chakula, sivyo?” **34** Yesu akawaambia: “Chakula changu ni kufanya mapenzi ya yule aliyenituma^c na kuimaliza kazi yake.”^d **35** Je, ninyi hamsemi kwamba bado kuna miezi minne kabla ya mavuno? Tazama! Ninawaambia: Inueni macho yenu mtazame mashamba, kwamba ni meupe kwa ajili ya kuvunwa.^e Tayari **36** mvunaji anapoeka mshahara na anakusanya matunda kwa ajili ya uzima wa milele, ili mpandaji na mvunaji washangilie pamoja.^f **37** Basi, maneno haya ni ya kweli: Mmoja ni mpandaji na mwingine ni mvunaji. **38** Niliwatuma mkavune kile ambacho hamkufanyia

kazi. Wengine wamefanya kazi, nanyi mmefaidika kutokana na kazi yao.”

39 Wasamaria wengi kuto-ka jiji hilo wakamwamini Yesu kwa sababu yule mwanamke alitoa ushahidi kwa kusema: “Aliniambia mambo yote niliyofanya.”^a **40** Basi Wasamaria walipomjia, wakamwomba akae pamoja nao, naye akakaa huko siku mbili. **41** Kwa hiyo, wengi zaidi wakaamini waliposikia mambo aliyosema, **42** nao wakamwambia yule mwanamke: “Hatuamini kwa sababu tu ya maneno yako; kwa maana sisi wenyewe tumesikia, na tuna-juu kwamba kwa hakika mtu huyu ndiye mwokozi wa ulimwengu.”^b

43 Baada ya siku hizo mbili akaondoka na kwenda Galilaya. **44** Hata hivyo, Yesu alitoa ushahidi kwamba nabii haheshimiwi katika nchi yake.^c **45** Kwa hiyo, alipofika Galilaya, Wagalilaya wakamkaribisha, kwa sababu walikuwa wameona mambo yote aliyofanya huko Yerusalemu kwenye sherehe,^d kwa maana wao pia walikuwa wameenda kwenye sherehe.^e

46 Kisha Yesu akaja tena Kana ya Galilaya, ambako alikuwa amegeuza maji kuwa divai.^f Basi kulikuwa na ofisa fulani wa mfalme ambaye mwana wake alikuwa mgonjwa huko Kapernaumu. **47** Mtu huyu aliposikia kwamba Yesu ametoka Yudea na kuja Galilaya, akamwendea na kumwomba ashuke kwenda kumpo-nya mwanawe, kwa maana alikuwa karibu kufa. **48** Lakini, Yesu akamwambia: “Msipoo-

SURA YA 4

a Yoh 4:29

b Mt 1:21
Yoh 1:29
ITI 1:15
IYo 4:14

c Mt 13:57
Mk 6:4
Lu 4:24

d Yoh 2:23

e Kum 16:16

f Yoh 2:1-11

Safu ya 2

a Mt 16:1
IKo 1:22

b Mt 8:13
Mk 7:29, 30

c Mt 8:13

d Yoh 2:11

SURA YA 5

e Kut 12:14
Kum 16:1, 16
Yoh 2:13
Yoh 6:4

f Ne 3:1

g Isa 53:3

na ishara na maajabu, hamtaamini kamwe.”^a **49** Yule ofisa wa mfalme akamwambia: “Bwana, twende kabla mwangu hajafa.” **50** Yesu akamwambia: “Rudi nyumbani; mwanao yuko hai.”^b Yule mtu akaamini maneno ambayo Yesu alimwambia, akaondoka. **51** Lakini akiwa njiani akakutana na watumwa wake, wakamwambia kwamba mwana-
we yuko hai.* **52** Kwa hiyo akawauliza saa ambayo alipata nafuu. Wakamjibu: “Alipona homa jana saa saba.”* **53** Kwa hiyo yule baba akajua ilikuwa saa ileile ambayo Yesu alimwambia: “Mwanao yuko hai.”^c Basi yeye na watu wote wa nyumbani kwake wakaaamini. **54** Huo ulikuwa muujiza wa pili^d ambao Yesu alifanya alipotoka Yudea na kwenda Galilaya.

5 Baada ya hayo kulikuwa na sherehe^e ya Wayahudi, na Yesu akapanda kwenda Yerusalemu. **2** Huko Yerusalemu kwenye Lango la Kوندoo^f kulikuwa na dimbwi lililoitwa kwa Kiebrania *Bethzatha*, lenye safu tano za nguzo. **3** Wagonjwa wengi, vipofu, vilema, na wenye viungo vilivyopooza walikuwa wamelala hapo. **4** *— **5** Lakini hapo palikuwa na mtu fulani aliye-kuwa mgonjwa kwa miaka 38. **6** Yesu alipomwona mtu huyo amelala hapo, na akijua kwamba alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu, akamuuliza: “Je, unataka kupona?”^g **7** Mgonjwa huyo akamjibu: “Bwana,

4:51 *Au “alikuwa anapata nafuu.”
4:52 *Yaani, karibu saa 7 mchana. 5:4
*Angalia Nyongeza A3.

sina mtu wa kuniweka ndani ya dimbwi maji yanapotibuliwa, lakini ninapotaka kuingia, mtu mwingine huingia kabla yangu.” **8** Yesu akamwambia: “Simama! Chukua mkeka wako,* utembe.”^a **9** Mtu huyo akapona mara moja, akabeba mkeka wake* na kuanza kutembea.

Hiyo ilikuwa siku ya Sabato. **10** Basi Wayahudi wakaanza kumwambia mtu huyo aliyeponywa: “Ni Sabato, hupaswi kubeba mkeka.”^b **11** Lakini akawajibu: “Yule aliyeniponya aliniambia, ‘Beba mkeka* wako utembee.’” **12** Wakamuuliza: “Ni nani huyo aliye kuambia, ‘Beba mkeka wako utembee?’” **13** Lakini mwanamume huyo aliyeponywa hakujua ni nani, kwa maana Yesu alikuwa ameingia katika umati uliokuwa hapo.

14 Baadaye, Yesu alimkuta hekaluni akamwambia: “Ona, sasa umepona. Usifanye dhambi tena, ili usipatwe na jambo baya zaidi.” **15** Yule mtu akaenda na kuwaambia Wayahudi kwamba Yesu ndiye aliyemponya. **16** Kwa hiyo Wayahudi walikuwa wakimtesa Yesu, kwa sababu alikuwa akifanya mambo hayo siku ya Sabato. **17** Lakini akawajibu: “Baba yangu anae ndelea kufanya kazi mpaka sasa, nami ninaendelea kufanya kazi.”^c **18** Basi Wayahudi wakazidi kutafuta njia ya kumuua, kwa sababu hakuwa tu akivunja Sabato bali pia alikuwa akimwita Mungu Baba yake,^d akijifanya kuwa sawa na Mungu.^e

5:8 *Au “kitanda chako.” 5:9 *Au “kitanda chake.” 5:10, 11 *Au “kitanda.”

SURA YA 5

a Mt 9:6
Mk 2:10, 11
Lu 5:24

b Kut 20:9, 10
Mt 12:2
Lu 6:2

c Yoh 9:4
Yoh 14:10

d Yoh 14:28

e Flp 2:5, 6

Safu ya 2

a Yoh 5:30
Yoh 8:28
Yoh 12:49

b Mt 3:17
Yoh 3:35
Yoh 10:17
2Pe 1:17

c Lu 8:25
Yoh 6:10, 11
Yoh 6:19

d 2Fa 4:32-34
Ebr 11:35

e Lu 7:12, 14
Lu 8:52-54
Yoh 11:25

f Mdo 10:42
Mdo 17:31
2Ko 5:10
2Ti 4:1

g Lu 10:16

h Yoh 3:16
Yoh 6:40
Yoh 8:51

i 1Yo 3:14

j Zb 36:9
Mdo 17:28

k Yoh 11:25

l Yoh 5:22
2Ti 4:1

19 Kwa hiyo, Yesu akawajibu: “Kwa kweli ninawaambia, Mwana hawezi kufanya hata jambo moja kwa uamuzi wake mwenyewe, ila tu lile analomwona Baba akifanya.”^a Kwa maana mambo yote ambayo Baba hufanya, vivyo hivyo Mwana hufanya mambo hayo. **20** Kwa maana Baba anampenda Mwana^b na humwonyesha mambo yote anayofanya, naye atamwonyesha kazi kubwa kuliko hizi, ili ninyi mshangae.^c **21** Kwa maana kama vile Baba anavyowafuwa wafu na kuwafanya kuwa hai,^d ndivyo Mwana pia anavyowafanya kuwa hai wale anaotaka.^e **22** Kwa maana Baba hamhukumu mtu yeyote kamwe, bali amemkabidhi Mwana kazi yote ya kuhukumu,^f **23** ili wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Yeyote ambaye hamheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyemtuma.^g **24** Kwa kweli nina waambia, yeyote ambaye husikia neno langu na kumwamini Yule aliyenituma ana uzima wa milele,^h naye hahukumiki bali amevuka kutoka katika kifo na kuingia kwenye uzima.ⁱ

25 “Kwa kweli ninawaambia, saa inakuja, nayo imefika, ambapo wafu wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale ambao wamesikiliza wataishi. **26** Kwa maana kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake mwenyewe,^j ndivyo pia amemruhusu Mwana awe na uzima ndani yake mwenyewe.^k **27** Naye amempa mamlaka ya kuhukumu,^l

5:26 *Au “alivyo na zawadi ya uhai ndani yake mwenyewe.”

kwa sababu yeye ndiye Mwana wa binadamu.^a **28** Msi-shangazwe na jambo hili, kwa maana saa inakuja ambayo wote walio katika makaburi ya ukumbusho wataisikia sauti yake^b **29** na kutoka, wale waliotenda mema kwenye ufufuo wa uzima, na wale waliozoea kutenda maovu kwenye ufufuo wa hukumu.^c **30** Siwezi kufanya jambo lolote kwa uamuzi wangu mwenyewe. Kama vile ninavyosikia, ndivyo ninavyohukumu; na hukumu yangu ni ya uadilifu^d kwa sababu sitafuti mapenzi yangu mwenyewe, bali mapenzi ya yule aliyenituma.^e

31 "Ikiwa mimi peke yangu ndiye ninayetoa ushahidi juu yangu mwenyewe, ushahidi wangu si wa kweli.^f **32** Kuna mwingine anayetoa ushahidi kunihusu, nami ninajua ushahidi anaotoa kunihusu ni wa kweli.^g **33** Mmewatuma watu kwa Yohana, naye ametoa ushahidi kuhusu kweli.^h **34** Hata hivyo, sikubali ushahidi wa mwanadamu, bali ninasema mambo haya ili mwokolewe. **35** Mtu huyo alikuwa taa inayowaka na kung'aa, na kwa wakati mfupi mlikuwa tayari kufurahia sana mwangaza wake.ⁱ **36** Lakini nina ushahidi mkubwa kuliko wa Yohana, kwa maana kazi ambazo Baba yangu alinipa nitimize, yaani, kazi hizi ninazofanya zinatoa ushahidi kwamba Baba alinituma.^j **37** Naye Baba aliyenituma ametoa ushahidi kunihusu.^k Ninyi hamjasikia sauti yake wakati wote wala kuona umbo lake,^l **38** nanyi hamna neno lake ndani yenu, kwa sa-

SURA YA 5

a Da 7:13

b Ayu 14:13
Isa 25:8
Isa 26:19

c Ufu 20:12, 15

d Isa 11:4

e Mt 26:39
Yoh 4:34
Yoh 6:38

f Kum 19:15

g Mt 3:17
Mk 9:7
Yoh 12:28-30
1Yo 5:9

h Yoh 1:15, 32

i Mt 3:1, 5, 6
Mk 6:20j Mt 11:5
Yoh 3:2
Yoh 7:31
Yoh 10:25k Mk 1:11
Yoh 8:18l Kum 4:11, 12
Yoh 1:18
Yoh 6:46

Safu ya 2

a Lu 11:52

b Kum 18:15

c Isa 53:3
Yoh 1:11

d Yoh 12:42, 43

e Kum 31:26, 27
Yoh 7:19f Kum 18:15
Lu 24:44
Yoh 1:45

SURA YA 6

g Mt 14:13
Lu 9:10

h Mk 6:33

i Lu 9:11

j Yoh 2:13
Yoh 5:1

babu hammwamini yule ambaye alimtuma.

39 "Mnayachunguza Maandiko^a mkifikiri mtapata uzima wa milele kupitia Maandiko hayo; nayo* ndiyo yanayotoa ushahidi kunihusu.^b **40** Hata hivyo, hamtaki kuja kwangu^c ili mpate uzima. **41** Mimi sikubali utukufu kutoka kwa wanadamu, **42** lakini ninajua kwamba hamna upendo wa Mungu ndani yenu. **43** Nimekuja katika jina la Baba yangu, lakini hamnikubali. Ikiwa mtu mwingine angekuja kwa jina lake mwenyewe, mngemkubali. **44** Mnawezaje kuniamini, huku mkipeana utukufu ninyi wenyewe lakini hamtafuti utukufu unaotoka kwa Mungu wa pekee?^d **45** Msifikiri kwamba nitawashtaki kwa Baba. Kuna yule anayewashtaki, Musa,^e ambaye mmeweka tumaini lenu kwake. **46** Kwa kweli, ikiwa mngemwamini Musa mngenihamini pia, kwa sababu aliandika kunihusu.^f **47** Lakini ikiwa hamwamini mambo aliyoandika, mnawezaje kuamini mambo ninayosema?"

6 Baada ya hapo Yesu akavuka Bahari ya Galilaya, au Tiberia.^g **2** Na umati mkubwa sana ulikuwa ukimfuata,^h kwa sababu walikuwa wakiona ishara za miujiza alizokuwa akifanya kwa kuwaponya wagonjwa.ⁱ **3** Basi Yesu akapanda mlimani, akaleti huko pamoja na wanafunzi wake. **4** Sasa Pasaka,^j ile Sherehe ya Wayahudi, ilikuwa imekaribia. **5** Yesu alipoinua macho yake na kuona

5:39 * Yaani, Maandiko.

umati mkubwa ukija, akamuuliza Filipo: “Tutanunua wapi mikate ili watu hawa wale?”^a

6 Hata hivyo, aliuliza swali hilo ili kumjaribu, kwa maana alijua jambo alilokuwa karibu kufanya. **7** Filipo akamjibu: “Mikate ya dinari* 200 haiwezi kutosha hata tukimpa kila mmoja wao kipande kidogo.” **8** Mmoja wa wanafunzi wake aitwaye Andrea, ndugu ya Simoni Petro, akamwambia: **9** “Hapa kuna mvulana mdogo aliye na mikate mitano ya shayiri na samaki wawili wadogo. Je, hivi vitawatoshwa watu wengi hivi?”^b

10 Yesu akasema: “Wambieni watu waketi.” Basi mahali hapo palikuwa na nyasi nyingi, nao watu wakaketi, karibu wanaume 5,000.^c

11 Yesu akaichukua ile mikate, akatoa shukrani, kisha akawagawia wale waliokuwa wameketi hapo; pia akafanya vivyo hivyo na wale samaki wadogo, watu wote wakala na kushiba. **12** Waliposhiha akawaambia wanafunzi wake: “Kusanyeni vipande vilivyobaki, ili chochote kisipotee.” **13** Basi wakakusanya vipande vilivyobaki wakajaza vikapu 12 baada ya watu kula kutokana na ile mikate mitano ya shayiri.

14 Watu walipoona muujiza aliofanya, wakaanza kusema: “Kwa kweli huyu ndiye Nabii aliyepaswa kuja ulimwenguni.”^d **15** Kisha Yesu akijua walitaka kuja kumkamata wamfanye awe mfalme, akaondoka^e tena akaenda mlimani akiwa peke yake.^f

6:7 *Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 6

a Mt 14:14-17
Mk 6:35-38
Lu 9:12,13

b 2Fa 4:42-44

c Mt 14:19-21
Mk 6:39-44
Lu 9:14-17

d Kum 18:15, 18

e Yoh 17:16
Yoh 18:36

f Mt 14:23
Mk 6:45

Safu ya 2

a Mt 14:22

b Mk 6:47-51

c Mt 8:24
Mt 14:24-33

d Mt 14:27
Mk 6:50

e Mt 14:34

f Yoh 1:38

16 Ilipofika jioni, wanafunzi wake wakashuka kwenda baharini,^a **17** wakapanda mashua ili wavuke bahari kwenda Kapernaumu. Sasa giza lilikuwa limeingia na bado Yesu hakuwa pamoja nao.^b **18** Pia, bahari ikainza kuchafuka kwa sababu upepo mkali ulikuwa ukivuma.^c **19** Hata hivyo, walipokuwa wamepiga makasia umbali wa karibu kilomita tano au sita,* wakamwona Yesu akitembea juu ya bahari akiikaribia mashua, nao wakaogopa. **20** Lakini akawaambia: “Ni mimi; msioogope!”^d **21** Basi walitaka kumbeba Yesu kwenye mashua, na mara moja mashua ikafika kwenye nchi kavu mahali walipokuwa wakienda.^e

22 Siku iliyofuata umati wa watu waliokuwa wamebaki ng'ambo ya bahari hawakuona mashua yoyote hapo. Mashua ndogo ilikuwepo, lakini Yesu hakuwa amepanda kwenye mashua hiyo pamoja na wanafunzi wake, bali wanafunzi walikuwa wameondoka peke yao. **23** Hata hivyo, mashua kutoka Tiberia zikafika karibu na mahali ambapo walikula mikate baada ya Bwana kutoa shukrani. **24** Basi umati ulipoona kwamba Yesu na wanafunzi wake hawapo, wakapanda mashua zao wakaenda Kapernaumu kumtufuta Yesu.

25 Walipompata ng'ambo ya bahari wakamuuliza: “Rabi,^f ulifika hapa wakati gani?”

26 Yesu akawajibu: “Kwa kweli ninawaambia, hamnitafuti

6:19 *Tnn., “karibu stadia 25 au 30.” Angalia Nyongeza B14.

kwa sababu mliona ishara, bali kwa sababu mlikula mikate mkashiba.^a **27** Msifanye kazi kwa ajili ya chakula kinachoharibika, bali kwa ajili ya chakula kinachodumu kufikia uzima wa milele,^b ambacho Mwana wa binadamu atawapa ninyi; kwa maana Baba, Mungu mwenyewe, amemia muhuri wake wa kibali.^c

28 Basi wakamuuliza: "Tufanye nini ili tutimize kazi za Mungu?" **29** Yesu akawajibu: "Hii ndiyo kazi ya Mungu, kwamba mmwamini* yule aliyemtuma."^d **30** Basi wakamwambia: "Utafanya ishara gani,^e ili tuone na kukuamini? Unafanya kazi gani?" **31** Mababu zetu walikula mana nyikani,^f kama ilivyoandikwa: 'Aliwapa mkate kutoka mbinguni ili wale.'^g **32** Kisha Yesu akawaambia: "Kwa kweli ninawaambia, Musa hakuwapa mkate kutoka mbinguni, lakini Baba yangu anawapa mkate wa kweli kutoka mbinguni. **33** Kwa maana mkate wa Mungu ni yule anayeshuka kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima." **34** Kwa hiyo wakamwambia: "Bwana, tupe mkate huo sikuzote."

35 Yesu akawaambia: "Mimi ndio mkate wa uzima. Yeyote anayekuja kwangu hatapata njaa kamwe, na yeyote anayeniamini hatapata kiu kamwe.^h **36** Lakini kama nilivyowaambia, mmeniona na bado hamwamini.ⁱ **37** Wote anaonipa Baba watakuja kwangu, nami sitamfukuza kamwe yeyote anayekuja kwangu;^j **38** kwa maana sikushuka kutoka mbinguni^k kufanya ma-

6:29 *Au "mwonyeshe imani katika."

SURA YA 6

a Yoh 6:11

b Yoh 4:14
Yoh 17:3
Ro 6:23

c Mt 3:17
Mdo 2:22
2Pe 1:17

d Mdo 16:31
1Yo 3:23

e Mt 12:38
Mk 8:12
Yoh 2:18
1Ko 1:22

f Kut 16:15
Hes 11:7

g Zb 78:24
Zb 105:40

h Yoh 4:14
Yoh 7:37
Ufu 22:17

i Yoh 6:64

j Mt 11:28, 29
Yoh 17:6

k Yoh 3:13
Yoh 8:23, 42

Safu ya 2

a Mt 26:39
Yoh 5:30

b Yoh 5:28, 29
Ro 6:5

c Yoh 10:27, 28

d Yoh 11:24
Mdo 17:31
1Th 4:16
Ufu 20:12

e Yoh 6:33

f Mk 6:3

g Yoh 6:65

h Yoh 11:24

i Isa 54:13

j Kut 33:17, 20

k Mt 11:27
Lu 10:22
Yoh 1:18

l Yoh 3:16

m Yoh 6:33

n Yoh 6:31

penzi yangu, bali mapenzi ya yule aliyenituma.^a **39** Haya ndiyo mapenzi ya yule aliye-nituma, kwamba nisipoteze yeyote kati ya wote alionipa, bali niwafufue^b katika siku ya mwisho. **40** Kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Baba yangu, kwamba kila mtu anayemtambua Mwana na kumwamini awe na uzima wa milele,^c nami nitamfufua^d siku ya mwisho."

41 Kisha Wayahudi wakaa-nza kunung'unika kwa sababu alisema: "Mimi ndio mkate ulioshuka kutoka mbinguni."^e **42** Nao wakaanza kusema: "Je, huyu si Yesu mwana wa Yosefu, ambaye baba yake na mama yake tunawajua?^f Sasa anawezaje kusema, 'Nimeshuka kutoka mbinguni?'" **43** Yesu akawaambia: "Acheni kunung'unika miongoni mwenu. **44** Hakuna mtu anayeweza kuja kwangu isipokuwa Baba aliyenituma amvute,^g nami nitamfufua siku ya mwisho.^h **45** Imean-dikwa katika Manabii: 'Wote watafundishwa na Yehova.'ⁱ Kila mtu ambaye amemsikiliza Baba na kujifunza huja kwangu. **46** Hakuna mwanadamu yeyote ambaye amemwona Baba,^j ila yule aliyetoka kwa Mungu; huyo amemwona Baba.^k **47** Kwa kweli ninawaambia, yeyote anayeamini ana uzima wa milele.^l

48 "Mimi ndio mkate wa uzima.^m **49** Mababu zenu walikula mana nyikani na bado wakafa.ⁿ **50** Huu ndio mkate unaoshuka kutoka mbinguni, ili yeyote anayeula asife. **51** Mimi ndio mkate ulio hai ambao ulishuka kutoka mbi-

6:45 *Angalia Nyongeza A5.

nguni. Yeyote akila mkate huu ataishi milele; na kwa kweli, mkate nitakaotoa ni mwili wangu kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.”^a

52 Kisha Wayahudi wakaa-nza kubishana wakiulizana: “Mtu huyu anawezaje kutupatia mwili wake tule?” **53** Basi Yesu akawaambia: “Kwa kweli ninawaambia, msipokula mwili wa Mwana wa binadamu na kunywa damu yake, hamna uzima ndani yenu.”^b **54** Yeyote akila mwili wangu na kunywa damu yangu ana uzima wa milele, nami nitamfufua^c siku ya mwisho; **55** kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli na damu yangu ni kinywaji cha kweli. **56** Yeyote anayekula mwili wangu na kunywa damu yangu hubaki katika muungano nami, nami katika muungano naye.^d **57** Kama vile Baba aliye hai alivyonituma nami ninaishi kwa sababu ya Baba, vivyo hivyo yule anayekula mwili wangu, ataishi kwa sababu yangu.^e **58** Huu ndio mkate ulioshuka kutoka mbinguni. Si kama vile walivyokula mababu zenu na bado wakafa. Yeyote anayekula mkate huu ataishi milele.”^f **59** Alisema mambo haya alipokuwa akifundisha katika sinagogi* huko Kapernaumu.

60 Waliposikia hivyo, wengi kati ya wanafunzi wake wakasema: “Maneno hayo yanashua; ni nani anayeweza ku-yasikiliza?” **61** Lakini Yesu, akitambua kwamba wanafunzi wake walikuwa wakitung'unika kuhusu hilo, akawaambia: “Je, jambo hili lime-

6:59 *Au labda, “kusanyiko la watu wote.”

SURA YA 6

a Ebr 10:10

b Yoh 6:33

c Yoh 6:40
1Ko 15:51, 52
1Th 4:16

d Yoh 15:4

e Yoh 5:26
1Ko 15:22

f Yoh 6:51

Safu ya 2

a Yoh 3:13
Yoh 6:38
Yoh 8:23
Mdo 1:9

b Gal 6:8

c Kum 8:3
Mt 4:4d Mt 9:3, 4
Yoh 2:24, 25
Yoh 13:11

e Yoh 6:44

f Lu 9:62

g Mt 16:16
Mk 8:29h Yoh 6:63
Yoh 17:3

i Lu 9:20

j Lu 6:13

k Lu 22:3
Yoh 13:18l Mt 26:14, 15
Yoh 12:4

SURA YA 7

m Yoh 5:18

n Law 23:34

o Mt 12:46
Mk 6:3
Lu 8:19
Yoh 2:12
Mdo 1:14
Gal 1:19

wakwaza? **62** Basi, itakuwaje mtakapomwona Mwana wa binadamu akipanda kuru-di kule alikotoka?^a **63** Roho ndiyo inayotokeza uzima;^b mwili hauna faida hata kido-go. Maneno niliyowaambia ni roho na ni uzima.^c **64** Lakini kuna wengine kati yenu ambao hawaamini.” Kwa maana tangu mwanzo Yesu aliwajua wale ambao hawakuamini na yule ambaye angemsaliti.^d **65** Akaendelea kusema: “Ndiyo sababu nimewaambia, hakuna mtu anayeweza kuja kwangu isipokuwa aruhusiwe na Baba.”^e

66 Kwa sababu hiyo, wengi kati ya wanafunzi wake wakarudi kwenye mambo yaliyo nyuma^f nao hawakumfuata tena. **67** Basi Yesu akawauli-za wale 12: “Je, ninyi pia mnataka kwenda?” **68** Simoni Petro akamjibu: “Bwana, tutaenda kwa nani?^g Wewe una maneno ya uzima wa milele.^h **69** Tumeamini na tumejua kwamba wewe ndiye Mtakati-fu wa Mungu.”ⁱ **70** Yesu akawaambia: “Niliwachagua ninyi 12, sivyo?^j Lakini mmoja wenu ni mchongezi.”^k **71** Kwa kweli, alikuwa akizungumza kumhusu Yuda mwana wa Simoni Iskariote, ambaye angemsaliti, ingawa alikuwa mmoja wa wale 12.^l

7 Baada ya mambo hayo Yesu aliendelea kusafiri* huko Galilaya, kwa maana hakutaka kwenda Yudea kwa sababu Wayahudi walitaka kumuua.^m **2** Hata hivyo, Sherehe ya Vibanda ya Wayahudi,ⁿ ilikuwa imekaribia. **3** Basi ndugu zake^o wakamwambia:

6:70 *Au “ibilisi.” **7:1** *Au “kutembea.”

“Ondoka hapa uende Yudea, ili wanafunzi wako pia wao ne kazi unazofanya. **4** Kwa maana mtu yeyote anayetaka kujulikana hadharani hafanyi jambo lolote kisiri. Ikiwa unafanya mambo haya jionyeshe kwa ulimwengu.” **5** Kwa kweli, ndugu zake hawakuwa wakimwamini.*^a **6** Basi Yesu akawaambia: “Bado wakati wangu haujafika,^b lakini wakati wenu upo sikuzote. **7** Ulimwengu hauna sababu ya kuwachukia ninyi, lakini unanichukia mimi kwa sababu ninatoa ushahidi kuuhusu kwamba matendo yake ni maovu.^c **8** Ninyi nendeni kwenye sherehe; mimi bado siendi kwenye sherehe hiyo, kwa sababu bado wakati wangu haujafika kikamili.”^d **9** Basi baada ya kuwaambia mambo hayo, akabaki Galilaya.

10 Lakini ndugu zake walipopanda kwenda kwenye sherehe, yeye pia alienda, lakini kisiri. **11** Basi Wayahudi wakaanza kumtafuta kwenye sherehe wakiuliza: “Yuko wapi yule mtu?” **12** Kulikuwa na minong’ono mingi kumhusu katika umati. Baadhi yao walisema: “Yeye ni mtu mwema.” Nao wengine wakasema: “Hapana. Anaupotosha umati.”^e **13** Bila shaka, hakuna mtu aliyesema waziwazi kumhusu kwa sababu waliwaogopa Wayahudi.^f

14 Sherehe ilipofika kati-kati, Yesu akapanda kuingia hekaluni na kuanza kufundisha. **15** Wayahudi wakashangaa na kuulizana: “Mtu huyu

7:5 *Au “wakionyesha kwamba wanamwamini.”

SURA YA 7

a Mk 3:21

b Yoh 2:4
Yoh 7:30

c Yoh 3:19
Yoh 15:19

d Yoh 8:20

e Yoh 9:16

f Yoh 9:22
Yoh 12:42
Yoh 19:38

Safu ya 2

a Lu 4:16, 17

b Mt 13:54
Mk 6:2
Lu 2:46, 47
Mdo 4:13

c Yoh 8:28
Yoh 12:49
Yoh 14:10

d Yoh 8:47

e Yoh 5:41
Yoh 8:50

f Kut 24:3

g Mt 12:14
Mk 3:6

h Law 12:2, 3

i Mwa 17:9, 10

j Yoh 5:8, 9

k Isa 11:3, 4
Mt 23:23

l Yoh 5:18

alipataje ujuzi wa Maandiko,*^a ingawa hajafundishwa shule-ni?”^{#b} **16** Naye Yesu akawaambia: “Mambo ninayofundisha si yangu, bali ni ya yule aliyenitama.^c **17** Mtu yeyote anayetamani kufanya mapenzi ya Mungu, atajua kama mafundisho haya yanatoka kwa Mungu^d au ninasema mambo niliyojitungia. **18** Mtu anayesema mambo aliyojitungia anajitafutia utukufu; lakini mtu anayetafuta utukufu wa yule aliye mtuma,^e huyo ni wa kweli, na hana ukosefu wowote wa uadilifu ndani yake. **19** Musa aliwapa Sheria,^f sivyo? Lakini hakuna yeyote kati yenu anayetii Sheria. Kwa nini mnataka kunia?”^g **20** Umati ukamwambia: “Wewe una roho mwovu. Ni nani anayetaka kukuu?” **21** Yesu akawajibu: “Nilifanya jambo moja tu, nyote mkashangaa. **22** Kwa hiyo Musa aliwapa tohara^h—si kwamba inatoka kwa Musa, bali inatoka kwa mababuⁱ—nanyi mnamtahiri mtu siku ya sabato. **23** Ikiwa mtu hutahiriwa siku ya sabato ili Sheria ya Musa isivunjwe, mbona mnanikasirikia sana kwa sababu nilimponya mtu siku ya sabato^j naye akapona kabisa? **24** Acheni kuhukumu kwa kutazama sura ya nje tu, bali hukumuni kwa uadilifu.”^k

25 Kisha baadhi ya wakaaji wa Yerusalemu wakaaanza kusema: “Huyu ndiye mtu wanayetaka kumuua, sivyo?” **26** Na bado oneni! anzungumza hadharani, na hawamwambii chochote. Je, kweli watawala wametambua kwa ha-

7:15 *Tnn., “maandishi.” #Yaani, shule za kirabi.

kika kwamba huyu ndiye Kristo? **27** Hata hivyo, tunajua mtu huyu ametoka wapi;^a lakini Kristo atakapokuja, hakuna mtu atakayejua alikotoka.” **28** Kisha Yesu alipokua akifundisha hekaluni akasema kwa sauti kubwa: “Ninyi mnanijua na pia mnajua nilikotoka. Nami sikuja kwa uamuzi wangu mwenyewe,^b lakini Yule aliyenituma ni halisi, nanyi hamujui.^c **29** Mimi ninamjua,^d kwa sababu mimi ni mwakilishi kutoka kwake, naye Ndiye aliyenituma.” **30** Basi wakaanza kutafuta njia ya kumkamata,^e lakini hakuna aliye-weza kumkamata, kwa sababu saa yake haukuwa imefika.^f **31** Hata hivyo, wengi katika umati walimwamini,^g nao wakaanza kusema: “Kristo atakapokuja, je, atafanya ishara nyingi kuliko alizofanya mtu huyu?”

32 Mafarisayo walisikia umati ukinong’onezana mambo hayo kumhusu, nao wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakawatuma maofisa wamkamata. **33** Kisha Yesu akasema: “Nitakuwa pamoja nanyi kwa muda mfupi kisha nitarudi kwa Yule aliyenituma.^h **34** Mtanitafuta lakini hamtanipata, na mahali nilipo hamwezi kuja.”ⁱ **35** Kwa hiyo, Wayahudi wakaanza kuulizana: “Mtu huyu anakusudia kwenda wapi, hivi kwamba hatutampata? Je, anakusudia kwenda kwa Wayahudi waliotawanyika kati ya Wagiriki ili awafundishe Wagiriki? **36** Anamaanisha nini anaposema, ‘Mtanitafuta, lakini hamtanipata, na mahali nilipo hamwezi kuja?’”

SURA YA 7

a Mt 13:55

b Yoh 8:42

c Yoh 8:54, 55

d Mt 11:27

Yoh 1:18

Yoh 10:15

e Mk 11:18

Lu 19:47

f Yoh 8:20

g Yoh 2:23

Yoh 8:30

Yoh 10:40, 42

Yoh 11:45

h Yoh 13:33

Yoh 16:16

i Yoh 8:21, 22

Safu ya 2

a Yoh 7:2

b Yoh 4:14

Yoh 6:35

c Kut 17:6

Hes 20:8

Yoh 4:14

d Yoe 2:28

Yoh 16:7

Mdo 2:17

e Yoh 12:16

Yoh 13:31, 32

1Ti 3:16

f Kum 18:18

Yoh 6:14

g Yoh 4:40, 42

Yoh 6:68, 69

h Yoh 1:46

Yoh 7:52

i 2Nya 13:5

Zb 89:3, 4

Zb 132:11

Yer 23:5

j Mik 5:2

Lu 2:4

k 1Sa 16:1

l Mt 7:28, 29

Lu 4:22

m Yoh 12:42

Mdo 6:7

37 Katika siku ya mwisho, siku kuu ya sherehe,^a Yesu alisimama na kusema kwa sauti kubwa: “Ikiwa yeyote ana kiu, na aje kwangu anywe maji.^b **38** Yeyote anayeniamini, kama andiko linavyosema: ‘Vijito vya maji ya uzi-ma vitatiririka kutoka ndani yake.’”^c **39** Hata hivyo, alikuwa akizungumza kuhusu roho, ambayo wale waliomwamini walikuwa karibu kupokea; kwa maana kufikia wakati huo hawakuwa wamepokea roho,^d kwa sababu bado Yesu hakuwa ametukuzwa.^e **40** Baadhi ya watu katika umati waliosikia maneno hayo wakaanza kusema: “Kwa kweli huyu ndiye Nabii.”^f **41** Wengine walikuwa wakisema: “Huyu ndiye Kristo.”^g Lakini wengine wakasema: “Kristo hatakuja kutoka Galilaya, sivyo?”^h **42** Je, andiko halisemi kwamba Kristo atatika katika uzao wa Daudi na atatika Bethlehemu,ⁱ kijiji alichoiishi Daudi?”^k **43** Basi kukatokea mgawanyiko kumhusu katika umati. **44** Hata hivyo, baadhi yao walitaka kumkamata, lakini hakuna yeyote aliyemkamata.

45 Kisha wale maofisa wakarudi kwa wakuu wa makuhani na Mafarisayo. Wakaauliza: “Kwa nini hamkumleta?” **46** Maofisa wakajibu: “Hakuna mtu mwingine yeyote ambaye amewahi kuzungumza hivyo.”^l **47** Nao Mafarisayo wakauliza: “Je, ninyi pia mmepotoshwa? **48** Je, kuna yeyote kati ya watawala au Mafarisayo ambaye amemwamini?”^m **49** Lakini umati huu usiojua Sheria ni watu

waliolaaniwa.” **50** Nikode-mo, aliyekuwa amemwendea hapo mwanzoni, na ambaye pia alikuwa mmoja wao akawaambia: **51** “Kulingana na Sheria yetu, kabla ya kumhukumu mtu, tunapaswa kumsikiliza ili tujue anachofanya, sivyo?”^a **52** Wakamjibu: “Je, wewe pia umetoka Galilaya? Chunguza uone kwamba hakuna nabii atakayeinuliwa kutoka Galilaya.”*

8 **12** Kisha Yesu akawaambia tena: “Mimi ndiye nuru ya ulimwengu.^b Yeyote anayenifuata hatatembea kamwe gizani, bali atakuwa na nuru^c ya uzima.” **13** Basi Mafarisayo wakamwambia: “Wewe unatoa ushahidi juu yako mwenyewe; ushahidi wako si wa kweli.” **14** Yesu akawajibu: “Hata ikiwa ninatoa ushahidi juu yangu mwenyewe, ushahidi wangu ni wa kweli, kwa sababu ninajua nilikotoka na ninakoenda.^d Lakini ninyi hamjui nilikotoka wala ninakoenda. **15** Ninyi mnahukumu kulingana na mwili;^e mimi simhukumu mtu yeyote kamwe. **16** Hata nikhukumu, hukumu yangu ni ya kweli, kwa sababu siko peke yangu, bali Baba aliyenituma yuko pamoja nami.^f **17** Pia, katika Sheria yenu imeandikwa: ‘Ushahidi wa watu wawili ni wa kweli.’^g **18** Mimi ninatoa ushahidi juu yangu mwenyewe, na Baba aliyenituma hutoa ushahidi kunihusu.”^h **19** Kisha wakamuuliza: “Baba yako yuko wapi?” Yesu akaji-

7:52 *Baadhi ya hati za kale zinazoamini- nika hazina mstari wa 53 hadi sura ya 8 mstari wa 11. 8:15 *Au “kwa viwango vya wanadamu.”

SURA YA 7

a Kum 1:16,17

SURA YA 8

b Isa 9:2
Isa 49:6
Mt 4:16
Yoh 1:5
Yoh 12:35

c Yoh 12:46
1Pe 2:9
1Yo 2:8

d Yoh 7:28
Yoh 13:3
Yoh 16:28

e Yoh 7:24

f Yoh 14:10

g Kum 17:6
Kum 19:15

h Yoh 5:37
2Pe 1:17
1Yo 5:9

Safu ya 2

a Yoh 16:3

b Mt 11:27
Yoh 14:7

c Mk 12:41

d Yoh 7:30

e Yoh 8:24

f Yoh 7:34
Yoh 13:33

g Yoh 3:31
Yoh 16:28

h Yoh 18:19, 20

i Hes 21:8, 9
Da 7:13
Mt 26:64
Yoh 3:14
Yoh 12:32, 33
Gal 3:13

j Mt 27:54

k Yoh 5:19, 30

bu: “Ninyi hamnijui mimi wala Baba yangu.^a Kama mngeni- jua mimi, mngemjua Baba yan- gu pia.”^b **20** Alisema mane- no hayo katika chumba cha hazina^c alipokuwa akifundi- sha hekaluni. Lakini hakuna mtu aliyemkamata, kwa saba- bu saa yake haikuwa imefika.^d

21 Kwa hiyo, akawaambia tena: “Ninaenda zangu, na- nyi mtanitafuta, na bado mta- kufa katika dhambi zenu.^e Ni- nakoenda hamwezi kuja.”^f

22 Basi Wayahudi wakaanza kuulizana: “Je, atajiua? Kwa sababu anasema, ‘Ninakoenda hamwezi kuja.’” **23** Akae- ndelea kuwaambia: “Ninyi mnatoka katika makao ya chi- ni; mimi ninatoka katika ma- kao ya juu.^g Ninyi mnatoka ka- tika ulimwengu huu; mimi si- toki katika ulimwengu huu.

24 Ndiyo maana niliwaambia: Mtakufa katika dhambi zenu. Kwa maana msipoamini kwa- mba mimi ndiye, mtakufa ka- tika dhambi zenu.” **25** Kwa hiyo wakaanza kumuuliza: “Wewe ni nani?” Yesu akawaji- bu: “Kwa nini hata ninazungu- mza nanyi? **26** Nina mambo mengi ya kusema kuwahusu na mengi ya kuhukumu. Kwa hakika, Yule aliyenituma ni wa kweli, na mambo niliyoya- sikia kutoka kwake ninayase- ma ulimwenguni.”^h **27** Hawa- kuelewa kwamba alikuwa aki- waambia kumhusu Baba.

28 Kisha Yesu akasema: “Baa- da ya kumwinua Mwana wa binadamu,ⁱ ndipo mtakapo- jua kwamba mimi ndiye/ na kwamba sifanyi jambo lolote kwa uamuzi wangu mwe- nyewe;^k bali mambo ambayo Baba amenifundisha, ndiyo

ninayosema. **29** Na Yule aliyenituma yuko pamoja nami; naye hakuniacha peke yangu, kwa sababu sikuzote mimi hufanya mambo yanayompendeza.”^a **30** Alipokuwa akisema mambo hayo, wengi wakamwamini.

31 Basi Yesu akawaambia Wayahudi waliokuwa wamemwamini: “Mkikaa katika neno langu, ninyi kwa kweli ni wanafunzi wangu, **32** nanyi mtaijua kweli,^b nayo kweli itawaweka ninyi huru.”^c

33 Wakamjibu: “Sisi ni uzao wa Abrahamu na hatujawahi kuwa watumwa wa mtu yeyote. Kwa nini basi unasema tutakuwa huru?” **34** Yesu akawajibu: “Kwa kweli ninawaambia, kila mtu anayetenda dhambi ni mtumwa wa dhambi.”^d

35 Isitoshe, mtumwa habaki nyumbani milele; lakini mwana hubaki milele. **36** Kwa hiyo, Mwana akiwaweka ninyi huru, kwa kweli mtakuwa huru. **37** Ninajua kwamba ninyi ni uzao wa Abrahamu. Lakini mnataka kuniua, kwa sababu neno langu halifanyi maendeleo kati yenu. **38** Ninasema mambo niliyoona nilipokuwa na Baba yangu,^e lakini ninyi mnafanya mambo mliyosikia kutoka kwa baba yenu.”

39 Wakamwambia: “Baba yetu ni Abrahamu.” Yesu akawaambia: “Kama mngekuwa watoto wa Abrahamu,^f mngefanya kazi za Abrahamu. **40** Lakini sasa mnataka kuniua, mimi ambaye nimewaambia kweli niliyosikia kutoka kwa Mungu.^g Abrahamu hakufanya hivyo. **41** Mnafanya kazi za baba yenu.” Wakamwambia: “Hatukuzaliwa kutokana na

SURA YA 8

a Yoh 4:34
Yoh 14:10
Ebr 1:9

b Yoh 17:17
Yoh 18:37

c Ro 6:14, 22
Yak 1:25

d Ro 6:6, 16
Ro 7:14

e Yoh 5:19

f Ro 2:28, 29
Ro 9:7, 8
Gal 3:7, 29

g Yoh 8:26

Safu ya 2

a Yoh 16:27
1Yo 5:1

b Yoh 3:16
Yoh 5:19, 30

c Mwa 3:15

d 1Yo 3:8

e Mwa 3:4
2Ko 11:3
Ufu 12:9

f Yoh 18:37

g Yoh 10:26
1Yo 4:6

h Yoh 4:9

i Mt 12:24
Yoh 7:20
Yoh 10:20

j Yoh 5:41
Yoh 7:18

uasherati;* tuna Baba mmoja tu, Mungu.”

42 Yesu akawaambia: “Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda,^a kwa maana nilitoka kwa Mungu nami nipo hapa. Sikuja kwa uamuzi wangu mwenyewe, bali Yeye ndiye aliyenituma.”^b

43 Kwa nini hamwelewi mambo ninayosema? Kwa sababu hamwezi kusikiliza neno langu. **44** Ninyi mmetoka kwa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kufanya tamaa za baba yenu.^c Alikuwa muuaji alipoanza,^{*d} naye hakusimama imara katika kweli, kwa sababu kweli haimo ndani yake. Anaposema uwongo, yeye husema kulingana na mwelekeo wake mwenyewe, kwa sababu yeye ni mwongo na ndiye baba ya uwongo.^e

45 Lakini kwa sababu mimi ninawaambia kweli, hamniamini. **46** Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? Ikiwa ninasema kweli, kwa nini hamniamini? **47** Yule anayetoka kwa Mungu husikiliza maneno ya Mungu.^f Kwa sababu hiyo, ninyi hamsikilizi, kwa kuwa hamtoki kwa Mungu.”^g

48 Wayahudi wakamjibu: “Je, hatusemi kweli tunaposema, ‘Wewe ni Msamaria’ na una roho mwovu?”ⁱ

49 Yesu akajibu: “Mimi sina roho mwovu bali ninamheshimu Baba yangu, lakini ninyi mnani-vunjia heshima. **50** Hata hivyo, mimi sijitafutii utukufu;^j kuna Yule anayetafuta na kuhukumu. **51** Kwa kweli

8:41 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. **8:44** *Au “tangu mwanzoni.”

ninawaambia, yeyote aki-shika maneno yangu, hatao-na kifo kamwe.”^a **52** Waya-hudi wakamwambia: “Sasa tu-najua una roho mwovu. Abra-hamu alikufa, na manabii vilevile, lakini wewe unase-ma, ‘Yeyote akishika mane-no yangu hataonja kifo ka-mwe.’ **53** Wewe si mkuu kuliko Abrahamu baba yetu ambaye alikufa, sivyo? Manabii pia walikufa. Unafikiri wewe ni nani?” **54** Yesu akajibu: “Ni-kijitukuza mwenyewe, utuku-fu wangu si kitu. Baba yangu ambaye mnasema ni Mungu wenu, ndiye anayenitukuza.”^b **55** Ninyi bado hamjamjua,^c la-kini mimi ninamjua.^d Kama ni-ngesema simjui, ningekuwa mwongo kama ninyi. Lakini mimi ninamjua, na ninalishi-ka neno lake. **56** Baba yenu Abrahamu alishangilia sana tazamio la kuona siku yangu, naye aliiona na kushangilia.”^e **57** Kisha Wayahudi wakamuuliza: “Wewe hujafika umri wa miaka 50, na bado umemwona Abrahamu?” **58** Yesu aka-waambia: “Kwa kweli nina-waambia, mimi nimekuwapo kabla Abrahamu hajakuwapo.”^f **59** Ndipo wakaokota mawe ili wampige, lakini Yesu akajificha na kuondoka he-kaluni.

9 Yesu alipokuwa akipita ali-mwona mtu aliyekuwa ki-pofu tangu kuzaliwa. **2** Ki-sha wanafunzi wake waka-muuliza: “Rabi,^g ni nani aliyetenda dhambi, ni mtu huyu au ni wazazi wake, hivi kwamba akazaliwa kipofu?” **3** Yesu akajibu: “Mtu huyu hakute-nda dhambi wala wazazi wake, bali ilikuwa hivyo ili kazi za Mungu zifunuliwe katika

SURA YA 8

a Yoh 5:24
Yoh 11:25, 26
1Ko 15:54
Ufu 20:6

b Yoh 5:41
Yoh 13:31, 32
Mdo 3:13

c Yoh 7:28

d Yoh 7:29

e Mt 13:17
Ebr 11:13

f Met 8:22
Yoh 17:5
Flp 2:6, 7
Kol 1:15-17

SURA YA 9

g Yoh 1:38

Safu ya 2

a Yoh 11:2-4

b Yoh 4:34
Yoh 11:9

c Isa 49:6
Isa 61:1
Yoh 1:5
Yoh 8:12

d Mk 8:23

e 2Fa 5:10, 14

f Yoh 9:7

g Yoh 9:6

h Lu 13:14
Yoh 5:8, 9

kisa chake.^a **4** Lazima tufa-nye kazi za Yule aliyenituma kukiwa bado mchana;^b usiku unakuja ambapo hakuna mtu atakayeweza kufanya kazi. **5** Maadamu nimo ulimwengu-ni, mimi ndiye nuru ya uli-mwengu.”^c **6** Baada ya kuse-ma mambo hayo, akatema mate chini akafanyiza tope kwa mate, na kumpaka mtu huyo kwenye macho^d **7** na kumwambia: “Nenda ukanawe katika dimbwi la Siloamu” (li-nalotafsiriwa kuwa “Aliyetu-mwa”). Naye akaenda na kuna-wa, akarudi akiwa anaona.^e

8 Basi majirani na watu wa-liokuwa wakimwona akiom-baomba wakaanza kuuliza-na: “Je, huyu si yule mtu aliye-kuwa akiketi akiombaomba?” **9** Baadhi yao walikuwa waki-sema: “Ni yeye.” Wengine wa-liukuwa wakisema: “Hapana, lakini anafanana naye.” Yule mtu akaendelea kusema: “Ni mimi.” **10** Basi wakamuuliza: “Macho yako yalifunguli-waje?” **11** Akajibu: “Mtu anayeitwa Yesu alifanyiza tope akanipaka kwenye ma-cho kisha akaniambia, ‘Ne-nda mpaka Siloamu ukanawe.’^f Basi nikaenda, nikanawa, nikaanza kuona.” **12** Ndipo wakamuuliza: “Yuko wapi mtu huyo?” Akasema: “Sijui.”

13 Wakampeleka kwa Mafa-risayo mtu huyo ambaye za-mani alikuwa kipofu. **14** Ika-wa kwamba siku ambayo Yesu alifanyiza tope na kuya-fungua macho ya mtu huyo^g ilikuwa Sabato.^h **15** Basi wa-kati huo Mafarisayo wakaa-nza kumuuliza jinsi alivyoa-nza kuona. Akawaambia: “Ali-nipaka tope kwenye macho yangu, nami nikanawa, sasa

ninaona.” **16** Kisha baadhi ya Mafarisayo wakaanza ku-sema: “Mtu huyo hatoki kwa Mungu, kwa sababu hashiki Sabato.”^a Wengine wakasema: “Mtenda dhambi anaweza kufanya ishara kama hizo?”^b Basi kukawa na mgawanyiko kati yao.^c **17** Wakamuuliza tena yule mtu aliyekuwa kipofu: “Unasemaje kumhusu kwa kuwa wewe ndiye uliyefunguliwa macho?” Akajibu: “Yeye ni nabii.”

18 Hata hivyo, Wayahudi hawakuamini kwamba alikuwa kipofu na sasa alikuwa anaona. Basi wakawaita wazazi wake **19** wakawauliza: “Je, huyu ni mwana wenu ambaye mnasema alizaliwa kipofu? Basi, imekuwaje kwamba sasa anaona?” **20** Wazazi wake wakajibu: “Tunajua kwamba huyu ni mwana wetu na alizaliwa akiwa kipofu. **21** Lakini hatujui jinsi alivyoanza kuona, wala hatujui mtu aliyemfungua macho. Muulizeni. Yeye ni mtu mzima. Anaweza kujieleza.” **22** Wazazi wake walisema hivyo kwa sababu waliogopa Wayahudi,^d kwa maana tayari Wayahudi walikuwa wamekubaliana kwamba mtu yeyote ambaye angemkiri kuwa ndiye Kristo, angefukuzwa katika sinagogi.^e **23** Ndiyo maana wazazi wake walisema: “Yeye ni mtu mzima, muulizeni.”

24 Basi wakamwita mara ya pili yule mtu aliyekuwa kipofu na kumwambia: “Mpe Mungu utukufu; tunajua mtu huyu ni mtenda dhambi.” **25** Akawajibu: “Kama yeye ni mtenda dhambi mimi sijui. Ninachojua ni kwamba nilikuwa kipofu,

SURA YA 9

a Kut 20:9,10

b Yoh 3:2

c Lu 12:51
Yoh 7:12, 43
Yoh 10:19d Yoh 7:13
Yoh 19:38e Yoh 12:42
Yoh 16:2

Safu ya 2

a Zb 66:18
Met 28:9
Isa 1:15b Zb 34:15
Met 15:29

c Yoh 5:36

d Yoh 9:22
Yoh 16:2

lakini sasa ninaona.” **26** Kisha wakamuuliza: “Alikufanyia nini? Aliyafunguaje macho yako?” **27** Akawajibu: “Tayari nimewaambia, lakini hamkusikiliza. Kwa nini mnataka kusikia tena? Je, ninyi pia mnataka kuwa wanafunzi wake?” **28** Ndipo wakawambia kwa dharau: “Wewe ni mwanafunzi wa mtu huyo, lakini sisi ni wanafunzi wa Musa. **29** Tunajua kwamba Mungu alizungumza na Musa; lakini mtu huyu, hatujui alikotoka.” **30** Yule mtu akawajibu: “Kwa kweli inashangaza kwamba hamjui alikotoka, ingawa ndiye aliyefungua macho yangu. **31** Tunajua kwamba Mungu hawasilizi watenda dhambi,^a lakini humsikiliza mtu yeyote anayemwogopa na kufanya mapeenzi yake.^b **32** Tangu zamani haijasikiwa kamwe mtu yeyote ameyafungua macho ya mtu aliyezaliwa kipofu. **33** Kama mtu huyu hakutoka kwa Mungu, hangeweza kufanya lolote.”^c **34** Wakamwambia: “Wewe ulizaliwa katika dhambi, na bado unajaribu kutufundisha?” Kwa hiyo, wakamfukuza!^d

35 Yesu akasikia kwamba walikuwa wamemfukuza mtu huyo. Basi alipompata akamuuliza: “Je, unamwamini Mwana wa binadamu?” **36** Yule mtu akauliza: “Bwana, huyu ni nani, niambie ili nimwamini?” **37** Yesu akawambia: “Tayari umemwona, na kwa kweli, yeye ndiye anayezungumza nawe.” **38** Akasema: “Ninamwamini, Bwana.” Naye akamsujudia.* **39** Kisha Yesu

9:38 *Au “akamwinamia.”

akasema: “Nilikuja ulimwengu kwa ajili ya hukumu hii, ili wale wasioona waweze kuona^a na wale wanaoona wawe vipofu.”^b **40** Baadhi ya Mafarisayo waliokuwa pamoja naye waliposikia mambo hayo wakamuuliza: “Je, sisi pia ni vipofu?” **41** Yesu akawaambia: “Kama mngekuwa vipofu, hamngekuwa na dhambi. Lakini sasa mnasema, ‘Tunaona.’ Dhambi yenu inabaki.”^c

10 “Kwa kweli ninawaambia, mtu asiyeingia katika zizi la kondoo kupitia mlango, bali anapanda na kuingia kupitia njia nyingine, ni mwizi na mporaji.^d **2** Lakini yule anayeingia kupitia mlango ndiye mchungaji wa kondoo.^e **3** Mlinzi wa mlango humfungulia,^f nao kondoo huisikiliza sauti yake.^g Naye huwaita kondoo wake kwa majina na kuwatoa nje. **4** Baada ya kuwatoa kondoo wake wote nje, yeye huwatangulia, nao kondoo humfuata kwa sababu wanaijua sauti yake. **5** Hawatamfuata mgeni kamwe bali watamkimbia, kwa sababu hawajui sauti ya wageni.” **6** Yesu aliwaambia mfano huo, lakini hawakuelewa alichokuwa akiwaambia.

7 Basi Yesu akasema tena: “Kwa kweli ninawaambia, mimi ndiye mlango wa kondoo.^h **8** Wote ambao wamekuja wakidai kwamba wao ni mimi, ni wezi na waporaji; lakini kondoo hawakuwasikiliza. **9** Mimi ndiye mlango; yeyote anayeingia kupitia kwangu ataokolewa, naye ataingia na kutoka na kupata malisho.ⁱ **10** Mwizi huja kuiba, kuua, na kuangami-

SURA YA 9

a Lu 4:18
Yoh 12:46

b Mt 11:25
Mt 13:13
Yoh 3:19

c Yoh 15:22

SURA YA 10

d Mt 7:15

e Mt 26:31
Mk 14:27
Yoh 10:11

f Lu 1:17
Yoh 3:28

g Yoh 10:27

h Yoh 14:6

i Yoh 21:17

Safu ya 2

a Mt 7:15

b Eze 34:23
Mt 9:36

c 1Sa 17:34, 35
Mt 20:28
Ebr 13:20

d Yoh 10:27

e Mt 11:27

f Mt 20:28
Yoh 15:13
1Yo 3:16

g Lu 12:32

h Eze 34:23
Eze 37:24
1Pe 5:4

i Yoh 17:23

j Isa 53:12
Flp 2:8
Ebr 2:9
Ebr 12:2

k Mdo 2:23, 24

l Lu 12:51
Yoh 7:12
Yoh 9:16

za.^a Mimi nimekuja ili wapate uzima na waupate kwa wingi. **11** Mimi ndiye mchungaji mwema;^b mchungaji mwema huutoa uhai wake* kwa ajili ya kondoo.^c **12** Mtu wa kuajiriwa, ambaye si mchungaji na ambaye kondoo si wake, anapomwona mbwamwitu aki-ja yeye huwaacha kondoo na kukimbia—naye mbwamwitu huwanyakua na kuwatawanya— **13** kwa sababu yeye ni mtu wa kuajiriwa naye hawajali kondoo. **14** Mimi ndiye mchungaji mwema. Ninawajua kondoo wangu nao kondoo wangu wanaijua,^d **15** kama Baba anavyonijua mimi, nami ninavyomjua Baba;^e na ninatoa uhai wangu* kwa ajili ya kondoo.^f

16 “Nami nina kondoo wengine, ambao si wa zizi hili;^g hao pia nitawaleta, nao wataisikiliza sauti yangu, nao watakuwa kundi moja, mchungaji mmoja.^h **17** Kwa sababu hiyo, Baba ananipenda,ⁱ kwa kuwa ninautoa uhai wangu*^j ili niupate tena. **18** Hakuna mtu anayeuchukua kutoka kwangu, bali ninautoa kwa hiari yangu. Nina mamlaka ya kuutoa, nami nina mamlaka ya kuupokea tena.^k Nilipokea amri hii kutoka kwa Baba yangu.”

19 Kisha mgawanyiko ukatokea tena kati ya Wayahudi^l kwa sababu ya maneno hayo. **20** Wengi wao walikuwa wakisema: “Ana roho mwovu naye ana wazimu. Kwa nini mnamsikiliza?” **21** Wengine wakasema: “Haya si maneno ya mtu mwenye roho mwovu. Je,

10:11 *Au “nafsi yake.” 10:15, 17 *Au “nafsi yangu.”

roho mwovu anaweza kufungua macho ya vipofu?”

22 Wakati huo kulikuwa na Sherehe ya Wakfu huko Yerusalemu. Ulikuwa wakati wa majira ya baridi kali, **23** na Yesu alikuwa akitembea hekaluni kwenye safu ya nguzo za Sulemani.^a **24** Kisha Wayahudi wakamzunguka na kuanza kumwambia: “Utae-ndelea kutuhangaisha* mpaka lini? Kama wewe ndiye Kristo, tuambie waziwazi.” **25** Yesu akawajibu: “Niliwaambia, na bado hamwamini. Kazi ninazofanya katika jina la Baba yangu, zinatoa ushahidi kunihusu.^b **26** Lakini hamwamini, kwa sababu ninyi si kondoo wangu.^c **27** Kondoo wangu husikiliza sauti yangu, nami ninawajua, nao hunifuata.^d **28** Mimi ninawapa uzima wa milele,^e nao hawataharibiwa kamwe, wala hakuna atakayewanyakua kutoka mkononi mwangu.^f **29** Kile ambacho Baba yangu amenipa ni chenye thamani kuliko vitu vingine vyote, na hakuna anayeweza kuwanyakua kutoka mkononi mwa Baba.^g **30** Mimi na Baba ni kitu kimoja.”**^h

31 Wayahudi wakaokota mawe tena ili wampige. **32** Yesu akawajibu: “Niliwaonyesha kazi nyingi nzuri kutoka kwa Baba. Kati ya kazi hizo, ni ipi inayofanya mtake kunipiga mawe?” **33** Wayahudi wakamjibu: “Tunakupiga mawe, si kwa sababu ya kazi njema, bali umekufuru;ⁱ kwa maana ingawa wewe ni mwanaadamu, unajifanya mungu.” **34** Yesu akawajibu: “Je, hai-

10:24 *Au “kuhangaisha nafsi zetu.”
10:30 *Au “tuna umoja.”

SURA YA 10

a Mdo 3:11

b Yoh 3:2
Yoh 5:36
Yoh 10:38
Yoh 14:10
Mdo 2:22

c Yoh 8:47

d Yoh 10:3

e Yoh 5:24
Yoh 17:1, 2f Yoh 6:37
Yoh 18:9

g 1Pe 1:4, 5

h Yoh 10:38
Yoh 17:11, 21

i Law 24:16

Safu ya 2

a Zb 82:6
1Ko 8:5

b Zb 82:1

c Lu 1:35
Yoh 5:18

d Yoh 5:36

e Yoh 14:10
Yoh 17:21

f Yoh 1:28

g Yoh 1:29

SURA YA 11

h Lu 10:38

i Mt 26:6, 7
Mk 14:3
Yoh 12:3

jaandikwa katika Sheria yenu, ‘Mimi nilisema: “Ninyi ni miungu”?’^a **35** Ikiwa aliwaita ‘miungu’^b wale ambao neno la Mungu lilikuja dhidi yao—na bado andiko halilwezi kubatilishwa— **36** je, mnaniambia mimi ambaye Baba alinitakasa na kunituma ulimwenguni, ‘Unakufuru,’ kwa sababu nilisema, ‘Mimi ni Mwana wa Mungu?’^c **37** Kama sifanyi kazi za Baba yangu, msiniamini. **38** Lakini ikiwa ninazifanya, hata ingawa hamniamini mimi, basi iweni na imani katika kazi hizo,^d ili mjue na kuendelea kujua kwamba Baba yuko katika muungano nami, nami niko katika muungano na Baba.”^e **39** Basi wakajiribu tena kumkamata; lakini akawakwepa.

40 Kisha akaenda tena ng’ambo ya Yordani mpaka mahali ambapo mwanzoni Yohana alikuwa akibatiza watu,^f naye akakaa huko. **41** Watu wengi wakamjia na kuanza kusema: “Yohana hakufanya ishara hata moja, lakini mambo yote aliyosema kumhusu mtu huyu yalikuwa ya kweli.”^g **42** Na watu wengi hapo wakamwamini Yesu.

11 Mtu fulani aliyemitwa Lazaro alikuwa mgonjwa; aliishi Bethania, giji cha Maria na Martha^h dada yake. **2** Huyu Maria ndiye aliyempaka Bwana mafuta yenye marashi na kufuta miguu yake kwa nywele zake;ⁱ Lazaro, ndugu yake ndiye aliye-kuwa mgonjwa. **3** Basi dada zake wakamtumia Yesu ujumbe wakisema: “Bwana, ona!

10:34 *Au “ni kama mungu.”

yule unayempenda ni mgonjwa.” **4** Lakini Yesu aliposikia hilo akasema: “Lengo la ugonjwa huu si kusababisha kifo, bali ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu,^a ili Mwana wa Mungu atukuzwe kupitia huo.”

5 Basi Yesu aliwapenda Martha na dada yake na Lazaro. **6** Hata hivyo, aliposikia kwamba Lazaro ni mgonjwa, Yesu aliendelea kukaa mahali alipokuwa kwa siku mbili zaidi. **7** Baada ya hayo, akawaambia wanafunzi: “Twendeni tena Yudea.” **8** Wanafunzi wakamwambia: “Rabi,^b juzijuzi tu Wayudea walitaka kukupiga mawe,^c nawe unarudi huko tena?” **9** Yesu akajibu: “Kuna saa 12 za mchana, sivyo?^d Yeyote akitembea mchana hatajikwaa, kwa sababu anaona mwangaza wa ulimwengu huu. **10** Lakini ikiwa yeyote anatembea usiku, atajikwaa kwa sababu hana nuru ndani yake.”

11 Baada ya kusema hayo, akawaambia: “Rafiki yetu Lazaro amelala usingizi,^e lakini ninasafiri kwenda huko ili kumwamsha.” **12** Kisha wanafunzi wakamwambia: “Bwana, ikiwa amelala usingizi, atapona.” **13** Hata hivyo, Yesu alikuwa akizungumza kuhusu kifo cha Lazaro. Lakini walifikiri anasema kuhusu kupumzika katika usingizi. **14** Ndipo Yesu akawaambia waziwazi: “Lazaro amekufa,^f **15** nami ninashangilia kwa ajili yenu kwamba sikuwapo, ili mwamini. Lakini twendeni kwake.” **16** Kwa hiyo Tomasi, aliyetitwa Pacha, akawaambia wanafunzi wenzake: “Sisi pia, twendeni tukafe pamoja naye.”^g

SURA YA 11

a Yoh 9:1-3

b Yoh 1:38

c Yoh 8:59
Yoh 10:31d Yoh 9:4
Yoh 12:35e Zb 13:3
Mt 9:24
Mdo 7:59, 60
IKo 15:6

f Mhu 9:5

g Yoh 11:8

Safu ya 2

a Lu 10:38, 39

b Isa 26:19
Yoh 5:28, 29
Mdo 24:15
Ebr 11:35
Ufu 20:12

c Yoh 14:6

d Yoh 8:51

e Mt 23:8
Yoh 13:13

17 Yesu alipofika, alikuta kwamba tayari Lazaro alikuwa kaburini* kwa siku nne. **18** Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu, umbali wa kilomita tatu hivi.* **19** Wayahudi wengi walikuwa wamekuja kwa Martha na Maria ili kuwafariji kwa sababu ya ku fiwa na ndugu yao. **20** Martha aliposikia Yesu anakuja, alienda kumlaki; lakini Maria^a alibaki nyumbani. **21** Kisha Martha akamwambia Yesu: “Bwana, kama ungekuwa hapa ndugu yangu hangekufa. **22** Lakini hata sasa ninajua kwamba chochote utakachomwomba Mungu, Mungu atakupa.” **23** Yesu akamwambia: “Ndugu yako atafufuka.” **24** Martha akamwambia: “Ninajua atafufuka katika ufufuo^b siku ya mwisho.” **25** Yesu akamwambia: “Mimi ndiye ufufuo na uzima.^c Yule anayeniamini, hata akifa, ataishi tena; **26** na kila mtu aliye hai na ananiamini hatakufa kamwe.^d Je, unaamini hilo?” **27** Akamwambia: “Ndiye Bwana, ninaniamini kwamba wewe ndiye Kristo, Mwana wa Mungu, yule anayekuja ulimwenguni.” **28** Baada ya kusema hayo, Martha akaenda kumwita Maria dada yake, akamwambia faraghani: “Mwalimu^e amefika naye anakuita.” **29** Aliposikia hilo, akasimama upesi, akamwendea.

30 Yesu hakuwa ameingia kijijini, bado alikuwa mahali alipokutana na Martha. **31** Wayahudi waliokuwa pamoja na Maria nyumbani wa-

11:17 *Au “kwenye kaburi la ukumbusho.” **11:18** *Tnn., “stadia 15 hivi.” Angalia Nyongeza B14.

kimfariji, walipomwona akisimama upesi na kuondoka, wakamfuata wakidhani kwamba alikuwa akienda kulia kwenye kaburi.*^a **32** Maria alipofika mahali alipokuwa Yesu na kumwona, akaanguka miguuni pake na kumwambia: "Bwana, kama ungekuwa hapa, ndugu yangu hangekufa." **33** Yesu alipomwona akilia na Wayahudi waliokuja pamoja naye wakilia pia, akaugua moyoni* na kutaabika. **34** Akauliza: "Mmemlaza wapi?" Wakamjibu: "Bwana, njoo uone." **35** Yesu akatokwa na machozi.^b **36** Ndipo Wayahudi wa-kaanza kusema: "Ona jinsi alivyompenda!" **37** Lakini baadhi yao wakauliza: "Je, mtu huyu aliyemfungua macho yule kipofu^c hangeweza ku-ziua huyu asife?"

38 Kisha baada ya Yesu kuugua tena moyoni, akaja kwenye lile kaburi.* Kwa kweli, lilikuwa pango lililofuni- kwa kwa jiwe. **39** Yesu akasema: "Liondoeni jiwe." Martha, dada ya yule aliyekufa akamwambia: "Bwana, kufikia sasa lazima awe ananuka, kwa maana ni siku nne." **40** Yesu akamwambia: "Je, sikukuambia kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?"^d **41** Basi wakaliondoa lile jiwe. Kisha Yesu akatazama mbinguni^e na kusema: "Baba, ninakushukuru kwa sababu umenisikia. **42** Kwa kweli, ninajua kwamba sikuzote wewe hunisikia; lakini nilisema kwa ajili ya umati waliosimama kunizunguka, ili waamini kwamba ulinitu-

11:31, 38 *Au "kaburi la ukumbusho."
11:33 *Tnn., "rohoni."

SURA YA 11

a Yoh 11:17

b Lu 19:41
Ebr 4:15

c Yoh 9:6, 7

d Yoh 9:1-3

e Mt 14:19
Mk 7:34, 35

Safu ya 2

a Yoh 12:28-30
Yoh 17:8

b Lu 7:12, 14

c Yoh 2:23
Yoh 10:42
Yoh 12:10, 11d Yoh 12:37
Mdo 4:15, 16e Mt 26:3
Lu 3:2
Mdo 4:5, 6

ma."^a **43** Baada ya kusema hayo, akaita kwa sauti kubwa: "Lazaro, njoo huku nje!"^b

44 Mtu huyo aliyekuwa amekufa akatoka, miguu na mikonoyake ikiwa imefungwa kwa vitambaa, na uso wake ikiwa umefungwa kwa kitambaa. Yesu akawaambia: "Mfungue- ni, mmwache aende."

45 Kwa hiyo, Wayahudi wengi waliokuwa wamekuja kwa Maria, wakamwamini Yesu walipoona alichofanya,^c

46 lakini baadhi yao wakae- nda kwa Mafarisayo na ku- waambia jambo ambalo Yesu alikuwa amefanya. **47** Basi wakuwa wakuhani na Ma- farisayo wakakusanya San- hdrini na kusema: "Tutafanya nini, kwa kuwa mtu huyu ana- fanya ishara nyingi?"^d **48** Tu- kimwacha aendelee, watu wote watamwamini, nao Wa- roma watakuja na kuchukua mahali petu* na taifa letu."

49 Lakini mmoja wao aitwa- ye Kayafa,^e aliyekuwa kuha- ni mkuu mwaka huo, akawa- mbia: "Ninyi hamjui chochote, **50** na hamwelewi kwamba ni kwa faida yenu mtu mmoja afe kwa ajili ya watu kuliko taifa lote liangamizwe." **51** Lakini hakusema hivyo kwa kujitu- ngia; bali kwa sababu alikuwa kuhani mkuu mwaka huo, ali- toa unabii kwamba Yesu ange- kufa kwa ajili ya taifa, **52** na si kwa ajili ya taifa tu, bali pia ili awakusanye watoto wa M- ngu waliotawanyika kotekote. **53** Basi tangu siku hiyo waka- panga njama ili kumuua.

54 Kwa hiyo, Yesu hakute- mbea tena hadharani kati ya Wayahudi, bali alienda katika

11:48 *Yaani, hekalu.

eneo lililo karibu na nyika, katika jiji linaloitwa Efraimu,^a naye akakaa huko pamoja na wanafunzi. **55** Sasa Pasaka^b ya Wayahudi ilikuwa karibu na watu wengi kutoka mashabani walipandani kwenda Yerusalemu kabla ya Pasaka ili wajitakase kisherehe. **56** Walikuwa wakimtafuta Yesu, nao wakawa wakiulizana wakiwa wamesimama hekaluni: “Mnaonaje? Je, kweli atakuja kwenye sherehe?” **57** Lakini wakuu wa makuhani na Mafarisayo walikuwa wametoa agizo kwamba ikiwa mtu yeyote angejua mahali alipo Yesu, alipaswa kuwajulisha ili wamkamate.

12 Siku sita kabla ya Pasaka, Yesu akafika Bethania, alikoishi Lazaro^c ambaye Yesu alikuwa amemfufua kutoka kwa wafu. **2** Basi, wakamwandalia mlo wa jioni huko, na Martha alikuwa akiwahudumia,^d lakini Lazaro alikuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakila* pamoja na Yesu. **3** Kisha Maria akachukua ratili* moja ya mafuta yenye marashi, nardo halisi, ghalii sana, akammimbia Yesu miguuni na kuifuta kwa nywele zake. Nyumba ikajaa harufu ya mafuta yenye marashi.^e **4** Lakini Yuda Iskariote,^f mmoja wa wanafunzi wake aliyekwa karibu kumsaliti akasema: **5** “Kwa nini mafuta haya yenye marashi hayangeuzwa kwa dinari* 300 na maskini wapewe pesa hizo?” **6** Hakusema hivyo kwa sababu aliwahangaikia maskini,

12:2 *Au “wameketi mezani.” 12:3 *Yaani, ratili ya Kiroma, karibu gramu 327. Angalia Nyongeza B14. 12:5 *Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 11

a 2Sa 13:23
2Nya 13:19

b Kut 12:14
Kum 16:1
Yoh 2:13
Yoh 5:1
Yoh 6:4
Yoh 12:1

SURA YA 12

c Yoh 11:1, 43

d Lu 10:40

e Mt 26:6-10
Mk 14:3-6

f Mt 26:47
Mk 14:10
Lu 22:48
Yoh 13:29
Mdo 1:16

Safu ya 2

a Mt 26:12
Mk 14:8
Yoh 19:40

b Kum 15:11

c Mt 26:11
Mk 14:7

d Yoh 11:43, 44

e Yoh 7:31
Yoh 11:44, 45

f Zb 118:25, 26

g Mt 21:8, 9
Mk 11:8, 9
Yoh 1:49

h Mt 21:7
Mk 11:7
Lu 19:35

i 1Fa 1:33, 34
Isa 62:11
Zek 9:9
Mt 21:5

j Yoh 7:39

bali kwa sababu alikuwa mwizi, naye ndiye aliyetunza sanduku la pesa na alikuwa akiba pesa zilizowekwa humo. **7** Kisha Yesu akawaambia: “Mwacheni afanye hivyo kwa ajili ya matayarisho ya siku ya mazishi yangu.”^a **8** Kwa maana maskini mnao sikuzote,^b lakini mimi hamtakuwa nami sikuzote.”^c

9 Wakati huohuo, umati mkubwa wa Wayahudi ukajua kwamba alikuwa huko, nao ukaja, si kwa sababu ya Yesu tu, bali pia ili kumwona Lazaro aliyekuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu.^d **10** Sasa wakuu wa makuhani wakapanga njama ili kumuua Lazaro pia, **11** kwa kuwa Wayahudi wengi walikuwa wakienda huko na kumwamini Yesu kwa sababu ya Lazaro.^e

12 Siku iliyofuata umati mkubwa uliokuwa umekuja kwenye sherehe, ukasi-ki kwamba Yesu alikuwa aki-ja Yerusalemu. **13** Basi wakachukua matawi ya mitende na kutoka nje kwenda kumlaki, nao wakaanza kusema kwa sauti kubwa: “Tunao- mba umwokoe! Amebariki- wa yule anayekuja katika jina la Yehova,”^f Mfalme wa Israeli!”^g **14** Yesu alipompa mwanapunda, akaketi juu yake,^h kama ilivyoandikwa: **15** “Usiogope binti ya Sayuni. Tazama! Mfalme wako anakuja, akiwa ameketi juu ya mwanapunda.”ⁱ **16** Mwanzoni, wanafunzi wake hawakuelewa mambo hayo, lakini Yesu alipotukuzwa,^j wakakumbuka kwamba mambo hayo yalikuwa yameandikwa kumhusu na

12:13 *Angalia Nyongeza A5.

kwamba walimtendea mambo hayo.^a

17 Umati uliokuwa pamoja naye alipomwita Lazaro kutoka kaburini^{*b} na kumfufua kutoka kwa wafu ukaendelea kutoa ushahidi.^c **18** Kwa sababu hiyo pia, umati ukanda kumlaki kwa sababu ulisikia alikuwa amefanya muujiza huo. **19** Basi Mafarisa-yo wakaambiana: “Mnaona, hamjafaulu hata kidogo. Tazama! Ulimwengu wote ume-mfuata.”^d

20 Sasa kulikuwa na baadhi ya Wagiriki miongoni mwa wale waliokuja kuabudu kwenye sherehe. **21** Basi, waka-mjia Filipo^e aliyetoka Bethsaida ya Galilaya, wakaanza kumwomba: “Bwana, tunataka kumwona Yesu.” **22** Filipo akaenda kumwambia Andrea, kisha wote wawili wakaja na kumwambia Yesu.

23 Lakini Yesu akawajibu: “Saa imefika ya Mwana wa binadamu kutukuzwa.^f **24** Kwa kweli ninawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka kwenye udongo na kufa, hubaki ikiwa mbegu moja tu; lakini ikifa,^g huzaa matunda mengi. **25** Yeyote anayeupenda sana uhai wake* huua-ngamiza, lakini yeyote anayeuchukia uhai wake^h katika ulimwengu huu ataulinda kwa ajili ya uzima wa milele.ⁱ **26** Ikiwa yeyote anataka kunihudumia, basi anifuata na mahali nilipo ndipo mhudumu wangu atakapokuwa pia.^j Ikiwa yeyote anataka kunihudumia, Baba atamheshimu.

12:17 *Au “kwenye kaburi la ukumbusho.” 12:25 *Au “anayeipenda sana nafsi yake.” ^aAu “anayeichukia nafsi yake.”

SURA YA 12

a Lu 24:45

Yoh 14:26

b Yoh 11:1, 43

c Mt 21:15

Lu 19:37

d Yoh 11:48

e Yoh 1:44

f Yoh 13:31, 32

Yoh 17:1

g Mt 16:21

Ro 14:9

1Ko 15:36

h Ufu 12:11

i Mt 16:25

Mk 8:35

Lu 9:24

j Yoh 14:3

Yoh 17:24

1Th 4:17

Safu ya 2

a Mt 26:38

Mk 14:34

b Lu 12:50

Lu 22:41, 42

Ebr 5:7

c Mt 3:17

Mt 17:5

Mk 1:11

Mk 9:7

Lu 3:22

Lu 9:35

2Pe 1:17

d Yoh 17:1

e Yoh 14:30

Yoh 16:11

Mdo 26:17, 18

2Ko 4:3, 4

Efe 2:1, 2

1Yo 5:19

f Lu 10:18

Ufu 12:9

g Yoh 8:28

h Mdo 5:30

i Zb 89:35, 36

Zb 110:4

Isa 9:7

j Yoh 3:14

k Yoh 11:10

l Efe 5:8

27 Sasa ninataabika,^{*a} nami niseme nini? Baba, niokoe kutoka katika saa hii.^b Hata hivyo, ndiyo sababu nimekuja kwenye saa hii. **28** Baba, litukuze jina lako.” Ndingo sauti^c ikasikika kutoka mbinguni ikisema: “Nimelitukuza nami nitalitukuza tena.”^d

29 Umati uliokuwa umesimama hapo ulisikia sauti hiyo ukaanza kusema kumekuwana na mngurumo. Nao wengine wakasema: “Malaika ameongea naye.” **30** Yesu akajibu: “Sauti hii imesikika, si kwa ajili yangu, bali kwa ajili yenu. **31** Sasa ulimwengu huu unahukumiwa; sasa mtawala wa ulimwengu^e huu atatupwa nje.^f **32** Na bado mimi, nikii-nuliwa kutoka duniani,^g nitawavuta watu wa namna zote kwangu.” **33** Kwa kweli alisema hivyo ili kuonyesha ni kifo cha aina gani alikuwa karibu kufa.^h **34** Kisha umati ukamwambia: “Tulisikia kutoka katika Sheria kwamba Kristo hudumu milele.ⁱ Kwa nini unasema kwamba lazima Mwana wa binadamu ainuliwe?^j Huyo Mwana wa binadamu ni nani?” **35** Basi Yesu akawaambia: “Nuru itakuwa miongoni mwenu kwa muda kidogo zaidi. Tembeeni wakati bado mna nuru, ili giza lisiwazidi nguvu; yeyote anayetembea katika giza hajui anakoenda.^k **36** Wakati mna nuru, iweni na imani* katika nuru ili muwe wana wa nuru.”^l

Yesu alisema mambo hayo, kisha akaenda kujificha mbali nao. **37** Ingawa alikuwa amefanya ishara nyingi

12:27 *Au “nafsi yangu inataabika.” 12:36 *Au “onyesheni imani.”

sana mbele yao, hawakuwa wakimwamini, **38** ili maneno haya aliyosema nabii Isaya yatimizwe: “Yehova,* ni nani ambaye ameamini jambo alilosikia kutoka kwetu?”^a Na mko-no wa Yehova,* umefunuliwa kwa nani?”^b **39** Wao hawakuamini kwa sababu pia Isaya alisema: **40** “Ame yapofusha macho yao naye ameifanya mioyo yao iwe migumu, ili wasione kwa macho yao na kuelewa kwa mioyo yao na kugeuka nami niwaponye.”^c **41** Isaya alisema mambo haya kwa sababu aliona utukufu wake, naye alisema kumhusu.^d **42** Hata hivyo, watawala wengi kwa kweli wali-mwamini,^e lakini hawakumkiri kwa sababu waliwaogopa Mafarisayo, ili wasifukuzwe katika sinagogi;^f **43** kwa maana waliupenda utukufu wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu.^g

44 Hata hivyo, Yesu akasema kwa sauti kubwa: “Yeyote anayeniamini, haniamini mimi tu bali pia Yule aliyenituma;”^h **45** na yeyote anayeniona mimi anamwona pia Yule aliyenituma.ⁱ **46** Nimekuja nikiwa nuru ulimwenguni,^j ili kila mtu anayeniamini asibaki gizani.^k **47** Lakini ikiwa yeyote anasikia maneno yangu na hayashiki, simhukumu; kwa maana sikuja kuuhukumu ulimwengu, bali kuuokoa.^l **48** Yeyote anayenipuuza na hapokei maneno yangu, ana wa kumhukumu. Neno ambalo nimesema ndilo litakalomhukumu katika siku ya mwisho. **49** Kwa maana

12:38 *Angalia Nyongeza A5. #Au “ujumbe wetu?”

SURA YA 12

a Ro 10:16

b Isa 53:1

c Isa 6:10
Mt 13:14
Mk 4:11, 12
Mdo 28:27

d Isa 6:1, 8

e Yoh 19:38

f Yoh 9:22
Yoh 16:2

g Yoh 5:44

h Mt 10:40
Mk 9:37

i Yoh 14:9

j Yoh 3:19
Yoh 8:12
Yoh 9:5

k Yoh 12:35

l Yoh 3:16, 17

Safu ya 2

a Yoh 8:38
Yoh 14:10

b Yoh 6:40

c Yoh 3:34

SURA YA 13

d Yoh 16:28
Yoh 17:11e Mt 26:2
Yoh 12:23
Yoh 17:1f Yoh 15:9
Efe 5:2
1Yo 3:16g Mt 26:14-16
Mt 26:24
Mk 14:10, 11h Lu 22:3, 4
Yoh 13:27

i Yoh 16:28

j Flp 2:5-7

k 1Ko 6:11
Efe 5:25, 26
Tit 3:5
Ebr 10:22

sijasema kwa uamuzi wangu mwenyewe, bali Baba aliyenituma amenipa amri kuhusu jambo la kutangaza na la kusema.^a **50** Pia, ninajua kwamba amri yake inamaanisha uzima wa milele.^b Kwa hiyo, mambo ninayosema, ninasema kama Baba alivyoniambia.”^c

13 Sasa, kwa sababu alijua kabla ya sherehe ya Pasaka kwamba saa yake ya kuondoka ulimwenguni na kwenda kwa Baba^d ilikuwa imefika,^e Yesu akiwa amewapenda walio wake ulimwenguni, aliwapenda mpaka mwisho.^f **2** Walipokuwa wakila mlo wa jioni, tayari Ibilisi alikuwa ameweka wazo la kumsaliti Yesu^g ndani ya moyo wa Yuda Iskariote,^h mwana wa Simoni. **3** Basi, Yesu akijua kwamba Baba alikuwa ameweka vitu vyote mikononi mwake na kwamba alikuja kutoka kwa Mungu na alikuwa akienda kwa Mungu,ⁱ **4** akasimama kutoka kwenye mlo wa jioni na kuyaweka baando mavazi yake ya nje. Naye akachukua taulo, akajifunga kiunoni.^j **5** Akatia maji kwenye beseni, akaanza kuiosha miguu ya wanafunzi na kuikausha kwa taulo aliyokuwa amejifunga kiunoni. **6** Kisha akamfikia Simoni Petro. Petro akamuuliza: “Bwana, unaoosha miguu yangu?” **7** Yesu akamjibu: “Ninalofanya huelewi sasa, lakini utaelewa baada ya mambo haya.” **8** Petro akamwambia: “Hutaosha kamwe miguu yangu.” Yesu akamjibu: “Nisipokuosha,^k wewe huna sehemu pamoja nami.” **9** Simoni Petro akamwambia: “Bwana, usioshe miguu ya-

ngu tu, bali pia mikono na kichwa changu.” **10** Yesu akamwambia: “Yeyote ambaye amega habitaji kuoshwa zaidi ya miguu yake, yuko safi kabisa. Nanyi mko safi, lakini sio nyote.” **11** Kwa maana alimjua mtu aliyekuwa akimsaliti.^a Ndiyo sababu alisema: “Sio nyote mlio safi.”

12 Baada ya kuosha miguu yao na kuvaa mavazi yake ya nje, akaketi mezani tena akawaambia: “Je, mnaelewa jambo ambalo nimewafanyia?”

13 Ninyi huniita, ‘Mwalimu,’ na, ‘Bwana,’ nanyi hamjako-sea, kwa maana ndivyo nilivyo.^b **14** Kwa hiyo, ingawa mimi ni Bwana na Mwalimu, niliiosha miguu yenu,^c basi ninyi pia mnapaswa* kuoshana miguu.^d **15** Kwa maana nimewawekea kielelezo, ili mfanye kama nilivyowafanyia.^e

16 Kwa kweli ninawaambia, mtumwa si mkuu kuliko bwana wake, wala yule aliyetumwa si mkuu kuliko yule aliyemtuma. **17** Ikiwa mnajua mambo haya, mtakuwa wenye furaha mkiyatenda.^f

18 Sisemi kuwahuu ninyi nyote; ninawajua wale ambao nimewachagua. Lakini ilikuwa hivyo ili andiko hili liti-mizwe:^g ‘Yule aliyekuwa akila mkate wangu amekiinua kisigino chake dhidi yangu.’^{*h}

19 Kuanzia sasa na kuendelea ninawaambia kabla jambo hilo halijatokea, ili litakapotokea mwamini kwamba mimi ndiye.ⁱ **20** Kwa kweli ninawaambia, yeyote anayempokea yule ninayemtuma ananipokea mimi pia,^j na yeyote

13:14 *Au “mna wajibu wa.” 13:18 *Au “amenigeuka.”

SURA YA 13

a Yoh 6:64

b Mt 23:8

c Lu 22:27

d Mt 20:26, 27

Lu 9:48

Lu 22:26

Ro 12:10

1Pe 5:5

e Flp 2:5

1Pe 2:21

1Yo 2:6

f Mt 7:24, 25

Lu 11:28

Yak 1:25

g Yoh 17:12

h Zb 41:9

Mt 26:23

i Yoh 14:29

Yoh 16:4

j Mt 25:40

Safu ya 2

a Mt 10:40

b Mt 26:21

Mk 14:18

Lu 22:21

Yoh 6:70

c Mt 26:22

Lu 22:23

d Yoh 19:26

Yoh 20:2

e Yoh 21:20

f Mt 26:23

g Lu 22:3, 4

h Yoh 12:4-6

i Mt 26:20

anayanipokea, anampokea pia Yule aliyenituma.”^a

21 Baada ya kusema mambo hayo, Yesu akataabika rohani, naye akatoa ushahidi akisema: “Kwa kweli ninawaambia, mmoja wenu atanisaliti.”^b **22** Wanafunzi wakaanza kutazamana, bila kujua alikuwa akisema kuhusu nani.^c **23** Mmoja wa wanafunzi ambaye Yesu alimpenda,^d alikuwa ameketi mezani karibu na* Yesu. **24** Kwa hiyo, Simoni Petro akamwonyesha huyo ishara kwa kichwa na kumwambia: “Tuambie anasema kuhusu nani.” **25** Basi mwanafunzi huyo akaegemea nyuma kifuani pa Yesu na kumuuliza: “Bwana, ni nani?”^e

26 Yesu akajibu: “Ni yule ambaye nitampa kipande cha mkate ninachochovya.”^f Basi, akachovya kipande cha mkate, kisha akampa Yuda, mwana wa Simoni Iskariote. **27** Baada ya Yuda kuchukua kipande hicho cha mkate, Shetani akamwingia.^g Kwa hiyo, Yesu akamwambia: “Kile unachofanya, kifanye upesi zaidi.” **28** Lakini hakuna hata mmoja kati ya wale waliokuwa wameketi mezani aliyejua kwa nini alimwambia hivyo. **29** Kwa kuwa Yuda alikuwa akitunza sanduku la pesa,^h baadhi yao walifikiri Yesu alikuwa akimwambia, “Nunua vitu tunavyohitaji kwa ajili ya sherehe,” au kwamba anapaswa kuwapa maskini kitu fulani. **30** Kwa hiyo, baada ya kupokea kipande cha mkate, mara moja akatoka nje. Ilikuwa usiku.ⁱ

13:23 *Tnn., “kifuani pa.”

31 Kwa hiyo alipoondoka, Yesu akasema: “Sasa Mwana wa binadamu ametukuzwa,^a na Mungu ametukuzwa kuhusiana naye. **32** Mungu mwenyewe atamtukuza,^b naye atamtukuza mara moja. **33** Watoto wadogo, nipo pamoja nanyi muda kidogo zaidi. Mtanitafuta; na kama nilivyo-waambia Wayahudi, ninawaambia ninyi pia, ‘Ninakoenda hamwezi kuja.’^c **34** Nina-wapa ninyi amri mpya, kwa-mba mpendane; kama vile ambavyo nimewapenda,^d nanyi mpendane vivyo hivyo.^e **35** Kwa jambo hili wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu—mkiwa na upendo miongoni mwenu.”^f

36 Simoni Petro akamuuliza: “Bwana, unaenda wapi?” Yesu akajibu: “Ninakoenda huwezi kunifuata sasa, lakini utanifuata baadaye.”^g **37** Petro akamwambia: “Bwana, kwa nini siwezi kukufuata sasa? Nitatoa uhai wangu* kwa ajili yako.”^h **38** Yesu akajibu: “Je, utatoa uhai wako* kwa ajili yangu? Kwa kweli ninakuambia, kabla ya jogoo kuwika utanikana mara tatu.”ⁱ

14 “Mioyo yenu isitaabike.^j Iweni na imani* katika Mungu;^k iweni na imani pia katika mimi. **2** Katika nyumba ya Baba yangu mna makao mengi. Kama sivyo, ningewaambia kwa maana ninaenda zangu kuwatayarishia mahali.^l **3** Pia, nikienda na kuwatayarishia mahali, nitakuja tena nami nitawapokea nyumbani

13:37 *Au “nafsi yangu.” 13:38 *Au “nafsi yako.” 14:1 *Au “Onyesheni imani.”

SURA YA 13

- a Yoh 12:23
- b Yoh 17:1
- c Yoh 7:34
Yoh 8:21
- d Yoh 15:9
- e Law 19:18
Yoh 15:12
1Th 4:9
Yak 2:8
1Pe 1:22
1Yo 3:14
- f Ro 13:8
1Ko 13:8, 13
1Yo 4:20
- g Yoh 14:3
- h Mt 26:33
Mk 14:29
Lu 22:33
- i Mt 26:34
Mk 14:30
Lu 22:34
Yoh 18:27

SURA YA 14

- j Yoh 14:27
- k Mk 11:22
1Pe 1:21
- l Lu 12:32
1Pe 1:3, 4

Safu ya 2

- a Yoh 17:24
Ro 8:17
Flp 1:23
1Th 4:16, 17
- b Yoh 11:16
- c Yoh 10:9
Efe 2:18
Ebr 10:19, 20
- d Yoh 1:17
Efe 4:21
- e Yoh 1:4
Yoh 6:63
Yoh 17:3
Ro 6:23
- f Mdo 4:12
- g Mt 11:27
Yoh 1:18
- h Yoh 12:45
Kol 1:15
Ebr 1:3
- i Yoh 10:38
Yoh 17:21
- j Yoh 7:16
Yoh 8:28
Yoh 12:49
- k Yoh 5:36
- l Mt 21:21
Mdo 1:8
Mdo 2:41
- m Mdo 2:32, 33

kwangu, ili mahali nilipo, ninyi pia muwe hapo.^a **4** Nanyi mnajua njia ya mahali nina-koenda.”

5 Tomasi^b akamwambia: “Bwana, sisi hatujui unakoenda. Tunawezaje kuijua njia?”

6 Yesu akamwambia: “Mimi ndiye njia^c na kweli^d na uzi-ma.^e Hakuna mtu anayekuja kwa Baba bila kupitia kwangu.^f **7** Kama ninyi mngeni-jua, mngemjua Baba yangu pia; tangu sasa na kuendelea ninyi mnamjua na mmemwona.”^g

8 Filipino akamwambia: “Bwana, tuonyeshe Baba na hilo linatutosha.”

9 Yesu akamwambia: “Je, hata baada ya kuwa pamoja nanyi kwa muda mrefu hivyo, bado Filipino hujanijua? Yeyote ambaye ameniona mimi amemwona Baba pia.^h Kwa nini unasema, ‘Tuonyeshe Baba?’

10 Je, huamini kwamba mimi nimo katika muungano pamoja na Baba, naye Baba yumo katika muungano pamoja nami?ⁱ Mambo ninayo-waambia sisemi kwa kujitungia,^j bali Baba ambaye hu-kaa katika muungano pamoja nami anafanya kazi zake.

11 Iweni na imani kwamba nimo katika muungano pamoja na Baba na Baba yumo katika muungano pamoja nami; kama sivyo, iweni na imani kwa sababu ya kazi zenyewe.^k

12 Kwa kweli ninawaambia, yeyote anayeniamini atafanya pia kazi ambazo mimi hufanya; naye atafanya kazi kubwa kuliko hizi,^l kwa sababu ninaenda zangu kwa Baba.^m

13 Pia, lolote mtakaloomba katika jina langu nitalifanya,

ili Baba atukuzwe kuhusiana na Mwana.^a **14** Mkiomba jambo lolote katika jina langu, nitalifanya.

15 "Ikiwa mnanipenda, mtazishika amri zangu.^b **16** Nami nitamwomba Baba, naye atawapa msaidizi* mwingine awe pamoja nanyi milele.^c **17** roho ya ile kweli,^d ambayo ulimwengu hauwezi kuipokea, kwa sababu hauioni wala kujua.^e Ninyi mnaijua, kwa sababu hiyo hukaa pamoja nanyi na imo ndani yenu. **18** Sitawaacha ninyi mayatima. Nina-kuja kwenu.^f **19** Bado muda kidogo nao ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mtaniona,^g kwa sababu ninaiishi, nanyi mtaishi. **20** Siku hiyo mtajua kwamba nimo katika muungano pamoja na Baba yangu nanyi mumo katika muungano pamoja nami, nami nimo katika muungano pamoja nanyi.^h **21** Yeyote aliyeniye na amri zangu na kuzishika, huyo ndiye anayenipenda. Na yeyote anayenipenda atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujionyesha waziwazi kwake."

22 Yuda,ⁱ sio Yuda Iskariote, akamuuliza: "Bwana, imekuwaje kwamba unakusudia kujionyesha waziwazi kwetu bali si kwa ulimwengu?"

23 Yesu akamjibu: "Ikiwa yeyote ananipenda, atalishika neno langu,^j naye Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na kukaa pamoja naye.^k **24** Yeyote asiyenipenda hayashiki maneno yangu. Neno mnalolisikia si langu, bali ni la Baba aliyenituma.^l

14:16 *Au "mfariji."

SURA YA 14

a Yoh 15:16
Yoh 16:23

b Yoh 13:34
Yoh 15:10
Yak 1:22

c Lu 24:49
Yoh 15:26
Yoh 16:7
Mdo 1:5
Mdo 2:1, 4
Ro 8:26

d Mt 10:19, 20
Yoh 16:13
1Ko 2:12
1Yo 2:27

e 1Ko 2:14

f Mt 28:20

g Mdo 10:40, 41

h Yoh 10:38
Yoh 17:21

i Lu 6:13, 16
Mdo 1:13

j Yoh 15:10

k 1Yo 2:24
Ufu 3:20

l Yoh 5:19
Yoh 7:16
Yoh 12:49

Safu ya 2

a Lu 24:49
Yoh 15:26
Yoh 16:13
1Yo 2:27

b Yoh 16:33
Efe 2:14
Flp 4:6, 7
Kol 3:15
2Th 3:16

c Yoh 20:17
1Ko 11:3
1Ko 15:28
Flp 2:5, 6

d Yoh 13:19
Yoh 16:4

e Yoh 12:31
Yoh 16:11

f Yoh 16:33

g Yoh 10:18
Yoh 12:49
Yoh 15:10
Flp 2:8

SURA YA 15

h 2Pe 1:8

i Yoh 13:10
Yoh 17:17

25 "Nimewaambia mambo haya nikiwa bado pamoja nanyi. **26** Lakini msaidizi, roho takatifu, ambayo Baba ataituma katika jina langu, hiyo itawafundisha mambo yote na kuwakumbusha mambo yote niliyowaambia.^a **27** Nina-waachia amani; ninawapa amani yangu.^b Siwapi amani kwa njia ile ambayo ulimwengu huitoa. Mioyo yenu isitaa-bike wala kuogopa. **28** Mlisikia nikiwaambia, 'Ninaenda, nami nitakuja tena kwenu.' Kama mngenipenda, mngeshangilia kwamba ninaenda kwa Baba, kwa maana Baba ni mkuu kuliko mimi.^c **29** Kwa hiyo sasa nimewaambia kabla jambo hilo halijatokea, ili litakapotokea mwamini.^d **30** Sitasema nanyi tena mambo mengi, kwa maana mtawala wa ulimwengu^e anakuja, naye hana uwezo juu yangu.^{*f} **31** Lakini, ili ulimwengu ujue kwamba ninampenda Baba, ninafanya kama vile Baba alivyonihamuru.^g Simameni tuondoke hapa.

15 "Mimi ndiye mzabibu wa kweli, naye Baba yangu ndiye mkulima. **2** Yeye huliondoa kila tawi ndani yangu lililozaa matunda, naye hulisafisha kila tawi linalozaa matunda, ili lizae matunda zaidi.^h **3** Tayari ninyi ni safi kwa sababu ya neno ambalo nimewaambia.ⁱ **4** Kaeni katika muungano pamoja nami, nami nitakaa katika muungano pamoja nanyi. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda likiwa peke yake lisipobaki katika mzabibu, vivyo hivyo hamwezi kuzaa matunda

14:30 *Au "hana nguvu juu yangu."

msipokaa katika muungano pamoja nami.^a **5** Mimi ndiye mzabibu; nanyi ndio matawi. Yeyote anayekaa katika muungano pamoja nami, nami katika muungano pamoja naye, huyo huzaa matunda mengi;^b kwa maana bila mimi hamwezi kufanya lolote kamwe. **6** Ikiwa yeyote hakai katika muungano pamoja nami, atatupwa kama tawi kisha atakauka. Nao watu hukusanya matawi hayo na kuyatupa ndani ya moto, nayo huteketea. **7** Mkikaa katika muungano pamoja nami, na maneno yangu yakae ndani yenu, ombeni chochote mna-
 chotaka nanyi mtapewa.^c **8** Baba yangu hutukuzwa kwa jambo hili, kwamba mwendeleo kuzaa matunda mengi na kujithibitisha kuwa wanafunzi wangu.^d **9** Kama vile Baba alivyonienda,^e ndivyo nimewapenda ninyi; kaeni katika upendo wangu. **10** Mkishika amri zangu, mtakaa katika upendo wangu, kama vile ambavyo nimeshika amri za Baba na kukaa katika upendo wake.

11 "Nimewaambia mambo haya, ili shangwe yangu iwe ndani yenu na shangwe yenu ijae.^f **12** Hii ndiyo amri yangu, kwamba mpendane kama vile nilivyowapenda.^g **13** Hakuna mtu aliye na upendo mkuu kuliko huu, kwamba mtu atoe uhai wake* kwa ajili ya rafiki zake.^h **14** Ninyi ni rafiki zangu ikiwa mnafanya mambo ninayo-
 waamuru.ⁱ **15** Siwaiti ninyi tena watumwa, kwa sababu mtumwa hajui mambo ambayo bwana wake hufanya. La-

15:13 *Au "nafsi yake."

SURA YA 15

a Yoh 6:56
 1Ko 12:27
 Efe 4:16

b Yoh 15:16

c Mt 7:7
 Yoh 16:23

d Mt 5:16
 Yoh 13:35
 Flp 1:9, 11

e Yoh 3:35

f Yoh 16:24
 Yoh 17:13

g Mk 12:31
 Yoh 13:34
 1Th 4:9
 1Pe 4:8

h Yoh 10:11
 Ro 5:7, 8
 Efe 5:1, 2
 1Yo 3:16

i Mt 12:50
 Yoh 14:23

Safu ya 2

a Yoh 14:13

b Yoh 13:34
 1Yo 3:23

c Mt 10:22
 Yoh 17:14

d Yak 4:4

e Lu 6:22
 Yoh 17:14
 1Pe 4:4

f Mt 5:11
 Mt 10:22
 Mt 24:9
 2Ti 3:12
 1Pe 2:21

g Yoh 16:2, 3

h Yoh 9:41

i Mt 11:21

j Yoh 5:23
 1Yo 2:23

k Mt 11:23
 Yoh 7:31
 Yoh 11:47

kini nimewaita rafiki, kwa sababu nimewajulisha mambo yote niliyosikia kutoka kwa Baba yangu. **16** Ninyi hamkunichagua, bali mimi niliwachagua na kuwaweka rasmi mwende na kuendelea kuzaa matunda na kwamba matunda yenu yadumu, ili hata mkimwomba Baba jambo lolote katika jina langu, awape.^a

17 "Mambo haya ninawaa-muru, kwamba mpendane.^b **18** Ikiwa ulimwengu unawachukia, kumbukeni kwamba umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi.^c **19** Kama mngekuwa sehemu ya ulimwengu, ulimwengu ungependa kilicho chake. Sasa kwa sababu ninyi si sehemu ya ulimwengu,^d bali nimewachagua kutoka ulimwenguni, kwa sababu hiyo ulimwengu unawachukia.^e **20** Kumbukeni neno nililowaambia: Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake. Ikiwa wamenitesa mimi, watawatesa ninyi pia;^f ikiwa wamelishika neno langu, watalishika lenu pia. **21** Lakini watawatendea mambo yote haya kwa ajili ya jina langu, kwa sababu hawamjui Yule aliyenitumba.^g **22** Kama singekuwa na kuzungumza nao, hawangukuwa na dhambi.^h Lakini sasa hawana kisingizio kwa ajili ya dhambi yao.ⁱ **23** Anayenichukia mimi anamchukia Baba/ yangu pia. **24** Kama singefanya kati yao kazi ambazo hakuna mwingine aliyezifanya, hawangukuwa na dhambi;^k lakini sasa wameniona, nao wamenichukia mimi na pia Baba yangu. **25** Lakini hilo lilifanyika ili kutimiza neno lililoandikwa ka-

tika Sheria yao: 'Walinichukia bila sababu.'^a **26** Atakapokuja msaidizi ambaye nitawatumia kutoka kwa Baba, roho ya ile kweli,^b inayotoka kwa Baba, huyo atatoa ushahidi kuhusu;^c **27** nanyi, mtatoa ushahidi,^d kwa sababu mme-kuwa pamoja nami tangu mwanzoni.

16 "Nimewaambia mambo haya ili msikwazike. **2** Watu watawafukuza kati-ka masinagogi.^e Kwa kweli, saa inakuja ambayo kila mtu atakayewaua^f atafikiri kwamba amemtolea Mungu utumishi mtakatifu. **3** Lakini watafanya mambo haya kwa sababu hawamjui Baba wala mimi.^g **4** Hata hivyo, nime-waambia mambo haya ili saa yake itakapofika, mkumbuke kwamba niliwaambia.^h

"Sikuwaambia mambo haya mwanzoni, kwa sababu nilikuwa pamoja nanyi. **5** Lakini sasa ninaenda kwa Yule aliye-nituma;ⁱ na bado hakuna hata mmoja wenu anayeniuliza, 'Unaenda wapi?' **6** Lakini kwa sababu nimewaambia mambo haya, mioyo yenu ime-jaa huzuni.^j **7** Hata hivyo, ninawaambia ukweli, ninaenda zangu kwa faida yenu. Kwa maana nisipoenda, msaidizi^k hatakuja kwenu; lakini ni-kienda, nitamtuma kwenu. **8** Naye atakapokuja atauthi-bitishia waziwazi ulimwengu kuhusu dhambi na kuhusu uadilifu na kuhusu hukumu: **9** kwanza kuhusu dhambi,^l kwa sababu hawaniamini;^m **10** kisha kuhusu uadilifu, kwa

16:9 *Au "hawaonyeshi kwamba wananiamini."

SURA YA 15

a Zb 35:19
Zb 69:4
Lu 23:22

b Lu 24:49
Yoh 14:26

c 1Yo 5:6

d Lu 24:48
Mdo 1:8
Mdo 2:22
Mdo 5:32

SURA YA 16

e Yoh 9:22

f Mt 24:9
Mdo 8:1
Mdo 12:1, 2
Mdo 26:11

g Yoh 8:19
Yoh 15:20, 21
Ro 10:2
1Ko 2:8

h Yoh 13:19
Yoh 14:29

i Yoh 7:33
Yoh 13:3

j Yoh 16:22

k Yoh 14:16, 26
Yoh 15:26
Mdo 2:32, 33

l Yoh 15:22

m Yoh 5:37, 38

Safu ya 2

a Yoh 12:31
Yoh 14:30

b Yoh 16:7

c Mdo 11:28
Mdo 21:10, 11
ITI 4:1

d 1Yo 4:2

e Yoh 15:26
1Yo 2:27

f Yoh 17:10

g Yoh 7:33
Yoh 14:19

sababu ninaenda kwa Baba nanyi hamtaniona tena; **11** pia kuhusu hukumu, kwa sababu mtawala wa ulimwengu huu amehukumiwa.^a

12 "Bado nina mambo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili kwa sasa. **13** Hata hivyo, huyo* atakapokuja, roho ya ile kweli,^b atawaongoza ninyi kwenye kweli yote, kwa maana hata-sema kwa uamuzi wake mwenyewe, bali atasema mambo anayosikia, naye atawatangazia mambo yanayokuja.^c **14** Huyo atanitukuza,^d kwa sababu atawatangazia mambo aliyopokea kutoka kwangu.^e **15** Vitu vyote alivyo navyo Baba ni vyangu.^f Ndiyo sababu nilisema huyo atawatangazia mambo aliyopokea kutoka kwangu. **16** Baada ya muda kidogo hamtaniona tena,^g na baada ya muda kidogo mtaniona."

17 Ndipo baadhi ya wanafunzi wake wakaulizana: "Anamaanisha nini anapotuambia, 'Baada ya muda kidogo hamtaniona, na tena, baada ya muda kidogo mtaniona,' na, 'kwa sababu ninaenda kwa Baba?'" **18** Basi walikuwa wakisema: "Anamaanisha nini anaposema, 'muda kidogo'? Hatuelewi anachozungumzia." **19** Yesu alijua kwamba walitaka kumuiliza, basi akawaambia: "Je, mnaulizana hivyo

16:13 *Maneno "huyo" na "naye" katika mstari wa 13 na 14 yanarejelea "msaidizi" aliyetajwa katika mstari wa 7. Yesu alitumia neno "msaidizi" (ambalo lina jinsia ya kiume katika Kigiriki) alipoipa roho takatifu sifa ya mtu ingawa ni nguvu isiyu na utu, na katika Kigiriki haina jinsia ya kiume wala ya kike.

kwa sababu nilisema: 'Baada ya muda kidogo hamtani-ona, na tena, baada ya muda kidogo mtaniona?' **20** Kwa kweli ninawaambia, mtalia na kuomboleza, lakini ulimwengu utashangilia; mtahuzunika, lakini huzuni yenu itageuka kuwa shangwe.^a **21** Mwanamke anapokuwa akizaa anahisi huzuni kwa sababu saa yake imefika, lakini baada ya kumzaa mtoto hakumbuki tena dhiki hiyo kwa sababu anashangilia kwamba mtu amezaliwa ulimwenguni. **22** Basi, ninyi pia mnahuzunika sasa; lakini nitawaona tena na mioyo yenu itashangilia^b na hakuna mtu atakayeondoa shangwe yenu. **23** Siku hiyo hamtaniuliza swali lolote. Kwa kweli ninawaambia, mkimwomba Baba jambo lolote,^c atawapa katika jina langu.^d **24** Kufikia sasa hamjaoomba hata jambo moja katika jina langu. Ombeni nanyi mtapewa, ili shangwe yenu iwe kamili.

25 "Nimewaambia mambo haya kwa mifano. Saa inakuja ambapo sitazungumza nanyi tena kwa mifano, bali nitawaeleza waziwazi kumhusu Baba. **26** Siku hiyo mtamwomba Baba katika jina langu; ninaposema hivyo, simaanshi kwamba nitawaombea ninyi. **27** Kwa maana Baba mwenyewe anawapenda ninyi, kwa sababu mmenipenda^e na mmeamini kwamba nilikuja nikiwa mwakilishi wa Mungu.^f **28** Nilikuja nikiwa mwakilishi wa Baba, nami nimekuja ulimwenguni. Sasa ninaondoka ulimwenguni, nami ninarudi kwa Baba."^g

SURA YA 16

- a Mt 28:8
Lu 24:39-41
Yoh 20:19, 20
- b Lu 24:51, 52
- c Flp 4:6
- d Yoh 14:13
Yoh 15:16
1Yo 5:14
- e Yoh 14:21
- f Yoh 17:7, 8
- g Yoh 13:3
Ebr 9:24

Safu ya 2

- a Zek 13:7
Mt 26:31
Mk 14:27
- b Yoh 8:29
- c Yoh 14:27
Efe 2:14
- d Yoh 14:30
Mdo 14:22
1Yo 4:4
1Yo 5:4
Ufu 3:21

SURA YA 17

- e Yoh 12:23
Yoh 13:31, 32
- f Flp 2:9, 10
- g Yoh 4:14
Yoh 6:27
- h Yoh 6:37
- i Lu 10:25-28
- j 1Yo 5:20
- k Efe 4:11, 13
2Pe 3:18
- l Yoh 13:31
- m Yoh 4:34
- n Yoh 1:1
Yoh 8:58
Kol 1:15
- o Zb 22:22
Mdo 15:14
Ebr 2:12

29 Wanafunzi wake wakanwambia: "Ona! Sasa unazungumza waziwazi, nawe hutumii mifano. **30** Sasa tunafahamu kwamba unajua mambo yote na huhitaji kuulizwa swali na mtu yeyote. Kwa hiyo, tunaamini kwamba ulitoka kwa Mungu." **31** Yesu akawajibu: "Je, sasa mnaamini? **32** Tazama! Saa inakuja, na kwa kweli imefika, wakati kila mmoja wenu atatawanyika na kwenda nyumbani kwake, nanyi mtaniacha peke yangu.^a Lakini siko peke yangu, kwa sababu Baba yuko pamoja nami.^b **33** Nimewaambia mambo haya ili kupitia kwangu muwe na amani.^c Ulimwenguni mtapata dhiki, lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu."^d

17 Yesu akasema mambo hayo, kisha akatazama mbinguni na kusema: "Baba, saa imefika. Mtukuze mwana wako ili mwana wako akutukuze,^e **2** kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili,^f ili awape uzima wa milele^g wote ambao umempa.^h **3** Uzima wa milele ndio huu,ⁱ wakujue wewe,^{*} Mungu wa pekee wa kweli,^j na yule uliyemtuma, Yesu Kristo.^k **4** Nimekutukiza dunia ni,^l kwa kuwa nimemaliza kazi uliyonipa nifanye.^m **5** Sasa Baba, nitukuze kando yako kwa utukufu niliokuwa nao kando yako kabla ya ulimwengu kuwako.ⁿ

6 "Nimelifunua* jina lako kwa watu ulionipa kutoka ulimwenguni.^o Walikuwa wako,

17:2 *Au "wanadamu wote; watu wote."

17:3 *Au "waendeleo kupata ujuzi juu yako wewe." 17:6 *Au "Nimelijulisha."

nawe ukanipa, nao wamelishika* neno lako. **7** Sasa wamejua kwamba vitu vyote ulivyonipa vimetoka kwako; **8** kwa sababu nimewapa maneno uliyonipa,^a nao wameyakubali na kwa hakika wamejua kwamba nilikuja nikiwa mwakilishi wako,^b nao wameamini kwamba ulinituma.^c **9** Ninaomba kwa ajili yao; siombi kwa ajili ya ulimwengu, bali ninawaomba wale ulionipa, kwa sababu ni wako; **10** na vitu vyangu vyote ni vyako na vyako ni vyangu,^d nami nimetukuzwa kati yao.

11 "Mimi simo tena ulimwenguni, bali wao wamo ulimwenguni,^e nami ninakuja kwako. Baba Mtakatifu, walinde^f kwa sababu ya jina lako ambalo umenipa, ili wawe kitu kimoja* kama vile sisi tulivyo kitu kimoja.^g **12** Nilipokuwa pamoja nao nilikuwa nikiwatunza^h kwa sababu ya jina lako ambalo umenipa; nami nimewalinda na hakuna hata mmoja wao aliyeangamizwaⁱ ila yule mwana wa maangamizi,^j ili andiko liti-mizwe.^k **13** Lakini sasa ninakuja kwako, nami ninasema mambo haya ulimwenguni ili wapate kikamili shangwe niliyo nayo.^l **14** Nimewapa neno lako, lakini ulimwengu umewachukia, kwa sababu wao si sehemu ya ulimwengu,^m kama vile ambavyo mimi si sehemu ya ulimwengu.

15 "Sikuombi uwatoe ulimwenguni, bali uwalinde kwa sababu ya yule mwovu.ⁿ **16** Wao si sehemu ya ulimwengu,^o kama vile amba-

17:6 *Au "wamelitii." 17:11 *Au "wawe na umoja." ^aAu "tulivyo na umoja."

SURA YA 17

a Yoh 6:68
Yoh 8:28
Yoh 12:49
Yoh 14:10

b Yoh 16:27

c Yoh 16:30

d Yoh 16:15

e Yoh 13:1

f 1Pe 1:5
Yud 24

g Yoh 10:30
Yoh 17:21

h Yoh 6:39
Yoh 10:28

i Yoh 18:9

j Mk 14:21

k Zb 41:9
Zb 109:8
Mdo 1:20

l Yoh 15:11

m Yoh 15:19
Yak 4:4

n Mt 6:13
2Th 3:3
1Yo 5:18

o Kol 1:13

Safu ya 2

a Yoh 18:36

b Efe 5:25, 26
1Th 5:23
2Th 2:13
1Pe 1:22

c Zb 12:6
Zb 119:151, 160

d Yoh 20:21

e Ro 12:5
1Ko 1:10
Gal 3:28

f Yoh 10:38
Yoh 14:10

g Yoh 14:20
Yoh 17:11
1Yo 3:24

h Lu 22:28-30
1Th 4:17

i Yoh 17:5

j Yoh 8:55
Yoh 15:21

k Mt 11:27

l Mt 6:9
Yoh 17:6

m Yoh 15:9

vyo mimi si sehemu ya ulimwengu.^a **17** Watakase* kupitia ile kweli;^b neno lako ni kweli.^c **18** Kama ulivyoni-tuma ulimwenguni, mimi pia nimewatuma ulimwenguni.^d **19** Nami ninajitakasa kwa ajili yao, ili wao pia watakaswe kupitia ile kweli.

20 "Ninaomba si kwa ajili ya hawa tu, bali pia wale wa-naoniamini kupitia neno lao, **21** ili wote wawe kitu kimoja,^e kama vile ambavyo wewe Baba umo katika muungano nami, nami nimo katika muungano nawe,^f ili wao pia wawe katika muungano nasi, ili ulimwengu uamini kwamba ulinituma. **22** Nimewapa utukufu ambao umenipa, ili wawe kitu kimoja kama vile sisi tulivyo kitu kimoja.^g **23** Mimi katika muungano nao nawe katika muungano nami, ili wakamilishwe wawe kitu kimoja,* ili ulimwengu ujue kwamba ulinituma na uliwapenda wao kama vile ulivyoni-penda. **24** Baba, ninataka wale ambao umenipa wawe pamoja nami mahali nilipo,^h ili waone utukufu wangu ambao umenipa, kwa sababu ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu.ⁱ **25** Baba Mwadilifu, kwa kweli, ulimwengu haujakujua wewe,^j lakini mimi ninakujua,^k na hawa wamejua kwamba ulinituma. **26** Nimewajulisha jina lako nami nitalijulisha,^l ili upendo ulionipenda uwe ndani yao nami katika muungano pamoja nao."^m

17:17 *Au "Uwaweke kando; Uwafanye wawe watakatifu." 17:23 *Au "waunganishwe kikamili."

18 Baada ya kusema mambo hayo, Yesu akaenda pamoja na wanafunzi wake, wakavuka Bonde la Kidroni*^a na kufika kwenye bustani, naye akaingia humo pamoja nao.^b **2** Sasa Yuda msaliti wake alijua mahali hapo, kwa sababu mara nyingi Yesu alikutana hapo na wanafunzi wake. **3** Basi Yuda akaja na kikosi cha wanajeshi, maofisa wa wakuu wa makuhani na wa Mafarisayo, wakafika hapo wakiwa na minge, taa, na silaha.^c **4** Kisha Yesu akijua mambo yote ambayo yangempata, akawakaribia na kuwauliza: “Mnamtafuta nani?” **5** Wakamjibu: “Yesu Mnazareti.”^d Akawaambia: “Ni mimi.” Basi Yuda msaliti wake, alikuwa pia amesimama pamoja nao.^e

6 Hata hivyo, Yesu alipo-waambia, “Ni mimi,” wakarudi nyuma na kuanguka chini.^f **7** Basi akawauliza tena: “Mnamtafuta nani?” Wakasema: “Yesu Mnazareti.” **8** Yesu akajibu: “Niliwaambia ni mimi. Basi, ikiwa mnanitafuta mimi, waacheni wanaume hawa waende.” **9** Hilo lilitimiza maneno aliyokuwa amesema: “Kati ya wale ulionipa, sikumpoteza hata mmoja.”^g

10 Simoni Petro alikuwa na upanga, basi akauchomoa na kumpiga mtumwa wa kuhani mkuu na kumkata sikio la kulia.^h Jina la mtumwa huyo lilikuwa Malko. **11** Hata hivyo, Yesu akamwambia Petro: “Rudisha upanga ndani ya ala yake.ⁱ Je, sipaswi kukinywa kikombe ambacho Baba amenipa?”^j

18:1 *Au “bonde la majira ya baridi kali la Kidroni.”

SURA YA 18

a 2Sa 15:23

b Mt 26:36
Mk 14:32
Lu 22:39c Mt 26:47
Mk 14:43

d Mt 2:23

e Lu 22:47

f Yoh 7:46

g Yoh 6:39
Yoh 17:12h Mt 26:51
Mk 14:47
Lu 22:50i Mt 26:52
Lu 22:51
Yoh 18:36j Mt 20:22
Mt 26:42

Safu ya 2

a Lu 3:2
Mdo 4:5, 6b Mt 26:57
Yoh 18:24

c Yoh 11:49, 50

d Mt 26:58
Mk 14:54
Lu 22:54e Mt 26:69, 70
Mk 14:66-68
Lu 22:55-57
Yoh 18:25f Mt 26:55
Lu 4:15
Lu 19:47
Yoh 7:14

12 Ndipo wanajeshi na kamanda wa jeshi na maofisa wa Wayahudi wakamkamata Yesu na kumfunga. **13** Kwanza wakampeleka kwa Anasi, kwa maana alikuwa baba mkwe wa Kayafa,^a ambaye alikuwa kuhani mkuu mwaka huo.^b **14** Kwa kweli, Kayafa ndiye aliyewashauri Wayahudi kwamba ilikuwa kwa faida yao mtu mmoja afe kwa ajili ya watu.^c

15 Sasa Simoni Petro na mwanafunzi mwingine wakamfuata Yesu.^d Mwanafunzi huyo alijulikana na kuhani mkuu, naye akaingia pamoja na Yesu ndani ya ua wa kuhani mkuu, **16** lakini Petro alikuwa amesimama nje kwenye mlango.* Basi yule mwanafunzi mwingine, aliyejulikana na kuhani mkuu, akatokea nje na kuzungumza na mlinzi wa mlango, akamwingiza Petro ndani. **17** Basi kijakazi, aliyekuwa mlinzi wa mlango, akamuuliza Petro: “Wewe pia ni mmoja wa wanafunzi wa mtu huyu, sivyo?” Petro akajibu: “Hapana.”^e **18** Sasa wale watumwa na maofisa walikuwa wamesimama kuzunguka moto wa makaa waliokuwa wameuwasha, kwa sababu kulikuwa na baridi nao walikuwa wakiota moto. Petro pia alikuwa amesimama pamoja nao akiota moto.

19 Basi mkuu wa makuhani akamuuliza Yesu kuhusu wanafunzi wake na kuhusu mafundisho yake. **20** Yesu akamjibu: “Nimezungumza na ulimwengu hadharani. Sikuzote nilifundisha katika sinagogi na hekaluni,^f ambapo Wayahu-

18:16 *Au “mwingilio.”

di wote hukusanyika, nami sikusema jambo lolote kwa siri. **21** Kwa nini unaniuliza? Waulize wale waliosikia nilichowaambia. Ona! Hawa wana-
 jua nilichosema.” **22** Baada ya kusema hivyo, mmoja wa maofisa aliyekuwa amesimama hapo karibu akampiga Yesu kofi usoni^a na kusema: “Je, hivyo ndivyo unavyomjibu mkuu wa makuhani?” **23** Yesu akamjibu: “Ikiwa nimesema vibaya, toa ushahidi kuhusu kosa hilo; lakini ikiwa nimesema jambo lililo sawa, kwa nini unanipiga?” **24** Kisha Anasi akaagiza Yesu apelekwe kwa kuhani mkuu Kayafa,^b akiwa amefungwa.

25 Sasa Simoni Petro alikuwa amesimama hapo akiota moto. Ndipo wakamwambia: “Wewe pia ni mmoja wa wanafunzi wake, sivyo?” Akakana na kusema: “Hapana.”^c **26** Mmoja wa watumwa wa kuhani mkuu, aliyekuwa mtu wa ukoo wa yule aliyekatawa sikio^d na Petro, akasema: “Nili kuona katika bustani pamoja naye, sivyo?” **27** Hata hivyo, Petro akakana tena, na papo hapo jogoo akawika.^e

28 Kisha wakamtoa Yesu kwa Kayafa na kumpeleka kwenye makao ya gavana.^f Ilikuwa asubuhi mapema. Lakini wao hawakuingia ndani ya makao ya gavana, ili wasitiwe unajisi^g kwa sababu walitaka kula mlo wa Pasaka. **29** Basi Pilato akatoka nje na kuwauliza: “Mna mashtaka gani kuhusu mtu huyu?” **30** Wakamjibu: “Kama mtu huyu hangekuwa mkosaji,^{*} hatunge mkabidhi kwako.” **31** Basi

SURA YA 18

a Isa 50:6

b Mt 26:57

c Mt 26:69, 70
Mk 14:69, 70
Lu 22:58

d Yoh 18:10

e Mt 26:74
Mk 14:72
Lu 22:60
Yoh 13:38f Mt 27:2
Mk 15:1
Lu 23:1

g Mdo 10:28

Safu ya 2

a Yoh 19:6

b Yoh 19:10

c Mt 20:18, 19
Yoh 3:14
Yoh 12:32d Mt 27:11
Yoh 12:13

e 1Ti 6:13

f Isa 9:6
Da 2:44
Da 7:14g Mt 26:52, 53
Yoh 18:11

h Mt 27:11

i Yoh 1:14, 17
Yoh 14:6j Mt 27:24
Lu 23:4
Yoh 15:25k Mt 27:15
Mk 15:6

Pilato akawaambia: “Mchukueni mkamhukumu kulingana na sheria yenu.”^a Wayahudi wakamwambia: “Si halali kwetu kumuua mtu yeyote.”^b **32** Hilo lilitimiza maneno aliyosema Yesu ili kuonyesha angekufa kifo cha aina gani.^c

33 Basi Pilato akaingia tena ndani ya makao ya gavana, akamwita Yesu na kumuuliza: “Je, wewe ndiye Mfalme wa Wayahudi?”^d

34 Yesu akajibu: “Je, unauliza hivyo kwa kujitungia, au uliambiwa na watu wengine kunihusu?” **35** Pilato akajibu: “Mimi si Myahudi, sivyo? Taifa lako na wakuu wa makuhani wamekukabidhi kwangu. Ulifanya nini?” **36** Yesu akajibu:^e “Ufalme wangu si sehemu ya ulimwengu huu.^f Kama Ufalme wangu ungekuwa sehemu ya ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi.^g Lakini, kama ilivyo, Ufalme wangu hautoki katika chanzo hiki.” **37** Basi Pilato akamuuliza: “Kwa hiyo, wewe ni mfalme?” Yesu akajibu: “Wewe mwenyewe unasema kwamba mimi ni mfalme.^h Nimezaliwa kwa ajili ya hili, na kwa ajili ya hili nimekuja ulimwenguni, ili nitoe ushahidi kuhusu kweli.ⁱ Kila mtu aliyepande wa kweli huisikiliza sauti yangu.” **38** Pilato akamuuliza: “Kweli ni nini?”

Baada ya kusema hivyo, akatoka nje tena na kuwambia Wayahudi: “Sijampata na kosa lolote.^j **39** Isitoshe, mna desturi kwamba niwafungulie mtu siku ya Pasaka.^k Basi, mnataka niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?”

40 Wakasema tena kwa sauti kubwa: “Si mtu huyu, bali Baraba!” Baraba alikuwa mwizi.^a

19 Kisha Pilato akamchukua Yesu, akampiga miyeledi.^b **2** Nao wanajeshi wakasokota taji la miiba kisha wakamvisha kichwani, pia wakamvisha joho la zambarau,^c **3** nao walikuwa waki-ja na kumwambia: “Salamu,* ewe Mfalme wa Wayahudi!” Pia walikuwa wakimpiga makofi usoni.^d **4** Pilato akatoka nje tena na kuwaambia: “Ona! Namtoa nje kwenu ili mjue kwamba sijampata na kosa lolote.”^e **5** Basi Yesu akatoka nje, akiwa amevaa taji la miiba na joho la zambarau. Naye Pilato akawaambia: “Tazama! Mwanamume!” **6** Hata hivyo, wakuu wa makuhani na maofisa walipomwona, wakasema kwa sauti kubwa: “Atundikwe mtini! Atundikwe mtini!”^f Pilato akawaambia: “Mchukueni mkamuue^g ninyi wenyewe, kwa maana mimi sijampata na kosa lolote.”^g **7** Wayahudi wakamjibu: “Sisi tuna sheria, na kulingana na sheria anapaswa kufa,^h kwa sababu alijifanya kuwa mwana wa Mungu.”ⁱ

8 Pilato aliposikia maneno yao, akaogopa hata zaidi, **9** akaingia tena ndani ya makao ya gavana akamuuliza Yesu: “Umetoka wapi?” Lakin Yesu hakumjibu.^j **10** Basi Pilato akamuuliza: “Unakataa kuzungumza nami? Je, hujui kwamba nina mamlaka ya kukufungua na mamlaka ya ku-

19:3 *Au “Uheshimiwe.” **19:6** *Au “Auawe kwenye mti! Auawe kwenye mti!”
^aAu “mkamuue kwenye mti.”

SURA YA 18

a Hes 35:31
 Lu 20:18, 19
 Mdo 3:14

SURA YA 19

b Isa 50:6
 Mt 20:18, 19
 Mt 27:26
 Mk 15:15

c Mt 27:27-29
 Mk 15:16, 17
 Lu 23:11

d Isa 53:3

e Lu 23:4
 Yoh 18:38

f Mt 27:22
 Mk 15:13
 Lu 23:21

g Yoh 18:31

h Law 24:16

i Mt 26:63-65
 Yoh 5:18

j Isa 53:7
 Mt 27:12, 14

Safu ya 2

a Lu 23:2
 Mdo 17:6, 7

b Yoh 19:31

c Da 9:26
 Mt 27:26, 31
 Mk 15:15
 Lu 23:24, 25

d Ebr 13:12

e Mt 27:32, 33
 Mk 15:22

f Yoh 3:14
 Mdo 5:30
 Gal 3:13

kuua?”* **11** Yesu akamjibu: “Wewe hungekuwa na mamla-ka yoyote juu yangu kama hungepewa kutoka juu. Ndiyo maana mtu aliyenitia mikononi mwako ana dhambi kubwa zaidi.”

12 Kwa sababu hiyo, Pilato akaendelea kutafuta njia ya kumfungua, lakini Wayahudi wakasema kwa sauti kubwa: “Ukimfungua mtu huyu, wewe si rafiki ya Kaisari. Kila mtu anayejifanya mfalme anasema vibaya kumhusu* Kaisari.”^a **13** Baada ya kusikia maneno hayo, Pilato akamtoa Yesu nje, naye akaketi kwenye kiti cha hukumu mahali panapoitwa Sakafu ya Jiwe, au katika Kiebrania, *Gabatha*. **14** Sasa ilikuwa siku ya Matayarisho^b ya Pasaka; karibu saa sita.* Naye akawaambia Wayahudi: “Oneni! Mfalme wenu!” **15** Hata hivyo, wakasema kwa sauti kubwa: “Mwondoe! Mwondoe! Atundikwe mtini!”* Pilato akawaambia: “Je, mnataka nimue mfalme wenu?” Wakuu wa makuhani wakajibu: “Sisi hatuna mfalme ila Kaisari.” **16** Kisha akamkabidhi kwao ili auawe kwenye mti.^c

Basi wakamchukua Yesu. **17** Yesu akabeba mti wake wa mateso,* akaenda mahali panapoitwa Fuvu la Kichwa,^d au *Golgotha* katika Kiebrania.^e **18** Hapo wakamtu-ndika mtini,^f na watu wawili kando yake, mmoja kulia na mwingine kushoto, naye

19:10 *Au “kukuua kwenye mti?” **19:12** *Au “anampinga.” **19:14** *Yaani, karibu saa 6 mchana. **19:15** *Au “Auawe kwenye mti!” **19:17** *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mti wa mateso.”

Yesu katikati yao.^a **19** Pilato akaandika pia tangazo na kuliweka juu ya huo mti wa mateso.* Liliandikwa: “Yesu Mnazareti Mfalme wa Wayahudi.”^b **20** Wayahudi wengi walilisoa tangazo hilo, kwa sababu mahali ambapo Yesu alitundikwa mtini palikuwa karibu na jiji, nalo liliandikwa katika Kiebrania, Kilatini, na Kigiriki. **21** Hata hivyo, wakuu wa makuhani wa Wayahudi wakamwambia Pilato: “Usiandike, ‘Mfalme wa Wayahudi,’ andika kwamba alisema, ‘Mimi ni Mfalme wa Wayahudi.’” **22** Pilato akajibu: “Yale ambayo nimeandika, nimeandika.”

23 Baada ya wanajeshi kumtundika Yesu kwenye mti, wakachukua mavazi yake ya nje na kuyagawanya vipande vinne, kila askari kipande kimoja, na pia wakachukua vazi la ndani. Lakini vazi la ndani halikuwa na mshono, lilikuwa limefumwa kutoka juu mpaka chini. **24** Basi wakaambiana: “Tusilirarue, badala yake tupige kura ili tuamue litakuwa la nani.”^c Hilo lilitimiza andiko linalosema: “Waligawana mavazi yangu, na wakalipigia kura vazi langu.”^d Kwa kweli, hivyo ndivyo walivyofanya wale wanajeshi.

25 Hata hivyo, kando ya mti wa mateso* wa Yesu, walikuwa wamesimama mama yake^e na dada ya mama yake; Maria mke wa Klopa na Maria Magdalene.^f **26** Basi, Yesu alipowona mama yake na mwanafunzi ambaye alimpenda^g wamesimama karibu, akamwa-

19:19, 25, 29 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 19

a Isa 53:9
Lu 23:33

b Mt 27:37
Mk 15:26
Lu 23:38

c Mt 27:35
Mk 15:24
Lu 23:34

d Zb 22:18

e Lu 2:34, 35

f Mt 27:55, 56
Mt 27:61
Mk 15:40
Lu 23:49

g Yoh 13:23
Yoh 21:7, 20

Safu ya 2

a Zb 22:15

b Zb 69:21
Mt 27:48
Mk 15:36
Lu 23:36

c Yoh 17:4

d Isa 53:12
Mt 27:50
Mk 15:37
Lu 23:46

e Yoh 19:14

f Kum 21:22, 23

g Law 23:5-7

h Isa 53:5
Zek 12:10
Yoh 20:25

i Yoh 20:31
Yoh 21:24

ambia mama yake: “Mwanamke, ona! Mwanao!” **27** Kisha akamwambia mwanafunzi huyo: “Ona! Mama yako!” Na tangu saa hiyo mwanafunzi huyo akamchukua Maria na kumpeleka nyumbani kwake.

28 Baada ya hayo, Yesu alipojua kwamba kufikia sasa mambo yote yalikuwa yametimizwa, akasema: “Nina kiu,”^a na hivyo akatimiza andiko. **29** Hapo palikuwa na chombo kilichojaa divai kali. Basi wakaweka sifongo iliyojaa divai kali juu ya kijiti cha hisopo* na kukileta karibu na mdomo wake.^b **30** Baada ya kuipokea ile divai kali, Yesu akasema: “Imetimizwa!”^c akainamisha kichwa chake akakata pumzi.^d

31 Kwa kuwa ilikuwa siku ya Matayarisho,^e ili miili hiyo isibaki kwenye miti ya mateso^f siku ya Sabato, (kwa maana siku hiyo ya Sabato ilikuwa kuu),^g Wayahudi walimwomba Pilato aagize miguu yao ivunjwe na miili iondolewe. **32** Basi, wanajeshi wakaja na kuvunja miguu ya wale watu wawili waliokuwa wametundikwa mtini kando ya Yesu. **33** Lakini walipomfikia Yesu, waliona kwamba tayari amekufa, kwa hiyo hawakuivunja miguu yake. **34** Lakini mwanajeshi mmoja akauchoma ubavu wa Yesu kwa mkuki,^h na mara moja damu na maji vikatoka. **35** Na yule aliyeona hilo ametoa ushahidi huu, nao ushahidi wake ni wa kweli, na anajua kwamba anachosema ni kweli, ili ninyi pia mwamini.ⁱ **36** Kwa kweli, mambo hayo

19:30 *Au “akafa.”

yalitendeka ili kutimiza andiko linalosema: “Hakuna mfu-pa wake hata mmoja utakaovunjwa.”*^a **37** Pia, andiko lingine linasema: “Watamtazama yule waliyemchoma.”^b

38 Baada ya mambo hayo Yosefu wa Arimathea, aliye-kuwa mwanafunzi wa Yesu la-kini kwa siri kwa sababu ali-waogopa Wayahudi,^c akamw-omba ruhusa Pilato ili auondoe mwili wa Yesu, naye Pilato akamruhusu. Basi akaja na kuuondoa mwili huo.^d **39** Ni-kodemo,^e yule mtu aliyemjia usiku mara ya kwanza, akaja pia akiwa amebeba mchanganyiko* wa manemane na udi, wenyewe uzito wa karibu ratili^f mia moja.^f **40** Basi wakau-chukua mwili wa Yesu na kuu-funga kwa vitambaa vya kita-ni pamoja na manukato,^g ku-lingana na desturi ya mazi-shi ya Wayahudi. **41** Ilitukia kwamba kulikuwa na bustani mahali alipouawa,* na katika bustani hiyo kulikuwa na ka-buri^{#h} jipya ambamo hakuna mtu alikuwa amewahi kula-zwa. **42** Kwa sababu iliku-wa siku ya Matayarisho/ ya Wayahudi na kaburi liliku-wa hapo karibu, wakamlaza Yesu humo.

20 Siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalene alienda mapema kwenye ka-buri,^{#i} kulipokuwa bado na giza, naye akaona jiwe li-meondolewa kwenye kabu-ri.^{#k} **2** Basi akakimbia kwe-

19:36 *Au “utakaopondwa.” 19:39 *Au labda, “mchanganyiko uliosokotwa.” #Yaani, ratili ya Kiroma. Angalia Nyo-ngeza B14. 19:41 *Au “alipouawa kwe-nye mti.” 19:41; 20:1 *Au “kaburi la ukumbusho.”

SURA YA 19

a Kut 12:46
Hes 9:12
Zb 34:20

b Zek 12:10
Ufu 1:7

c Yoh 7:13
Yoh 9:22

d Kum 21:22, 23
Mt 27:57-60
Mk 15:43-46

e Yoh 3:1, 2
Yoh 7:50-52

f Lu 23:55, 56

g Yoh 20:7

h Isa 53:9

i Yoh 19:14

SURA YA 20

j Mt 28:1
Mk 16:1, 2

k Lu 24:1-3

Safu ya 2

a Yoh 13:23
Yoh 19:26
Yoh 21:24

b Yoh 19:41, 42

c Yoh 19:40

d Zb 16:10
Mt 16:21
Mdo 2:27

e Mk 16:5

nda kwa Simoni Petro na yule mwanafunzi mwingine, amba-ye Yesu alimpenda,^a naye akawaambia: “Wamemwondoa Bwana kaburini,^b nasi hatujui wamemlaza wapi.”

3 Ndipo Petro na yule mwa-nafunzi mwingine wakaelekea kaburini. **4** Wote wawili wa-kaanza kukimbia pamoja, la-kini yule mwanafunzi mwingi-ne akakimbia upesi kuliko Pe-tro akatangulia kufika kwenye kaburi. **5** Akainama, akaona vitambaa vya kitani hapo chini,^c lakini hakuvingia ndani. **6** Ndipo Simoni Petro akaja akimfuata, akaingia kaburi-ni. Naye akaona vile vitambaa vya kitani hapo chini. **7** Ki-tambaa ambacho Yesu aliku-wa amefungwa kichwani ha-kikuwa pamoja na vitambaa vingine bali kilikuwa kime-kunjwa na kuwekwa kando. **8** Kisha yule mwanafunzi mwingine aliyetangulia kufi-ka kwenye kaburi akaingia pia, naye akaona na kuamini. **9** Kwa maana bado hawakuwa wameelewa andiko linalosema kwamba lazima afufuliwe ku-toka kwa wafu.^d **10** Basi wa-nafunzi hao wakarudi nyu-mbani kwao.

11 Hata hivyo, Maria akae-ndelea kusimama nje ya kaburi akilia. Alipokuwa aki-lia, akainama kutazama nda-ni ya kaburi, **12** naye akaona malaika wawili^e waliovaa mavazi meupe wakiwa wame-keti mahali ulipokuwa ume-lazwa mwili wa Yesu, mmo-ja kichwani na mwingine mi-guini. **13** Nao wakamuuliza: “Mwanamke, kwa nini una-lia?” Akawajibu: “Wamemwo-ndoa Bwana wangu, nami sijui

wamemlaza wapi.” **14** Baada ya kusema hayo, akageuka na kumwona Yesu akiwa amesimama hapo, lakini hakutambua kwamba ni Yesu.^a

15 Yesu akamuuliza: “Mwanamke, kwa nini unalia? Unamtafuta nani?” Maria, akifikiri kwamba ni mtunza-bustani, akamwambia: “Bwana, ikiwa umemchukua, niambie umemlaza wapi, nami nitamwondoa.” **16** Yesu akamwita: “Maria!” Alipogeuka akasema kwa Kiebrania: “*Rabonni!*” (maana yake “Mwalimu!”) **17** Yesu akamwambia: “Acha kuning’ang’ania, kwa maana bado sijapanda kwenda kwa Baba. Lakini nenda kwa ndugu zangu,^b nawe uwaambie, ‘Ninapanda kwenda kwa Baba yangu^c na Baba yenu na kwa Mungu wangu^d na Mungu wenu.” **18** Maria Magdalene akaenda na kuwaambia wanafunzi: “Nimemwona Bwana!” Kisha akawaambia alichoaambiwa na Yesu.^e

19 Ilipofika jioni siku hiyo, siku ya kwanza ya juma, milango ikiwa imefungwa mahali ambapo wanafunzi walikuwa kwa sababu ya kuwaogopa Wayahudi, Yesu akaja na kusimama katikati yao na kuwaambia: “Na muwe na amani.”^f **20** Baada ya kusema hayo, akawaonyesha mikono yake na ubavu wake.^g Basi wanafunzi wakashangilia walipomwona Bwana.^h **21** Yesu akawaambia tena: “Na muwe na amani.ⁱ Kama vile ambavyo Baba amenituma,^j mimi pia ninawatuma ninyi.”^k **22** Baada ya kusema hivyo akapuliza juu yao na kuwaambia: “Po-keeni roho takatifu.^l **23** Mki-

SURA YA 20

a Lu 24:15, 16
Lu 24:30, 31
Yoh 21:4

b Mt 28:10

c Yoh 14:28
Yoh 16:28

d 1Ko 11:3
Efe 1:17
Kol 1:3

e Lu 24:9, 10

f Lu 24:36

g Yoh 19:34

h Yoh 16:22

i Lu 24:36

j Isa 61:1
Yoh 5:36

k Mt 28:19, 20
Yoh 17:18

l Mdo 2:2, 4

Safu ya 2

a Yoh 11:16

b Yoh 19:34

c Yoh 20:19

d Yoh 21:25

e Yoh 3:15
Yoh 5:24
1Pe 1:8, 9
1Yo 5:13

msamehe mtu yeyote dhambi zake, atasamehewa; msipomsamehe mtu yeyote dhambi zake, hatasamehewa.”

24 Lakini Tomasi,^a mmoja wa wale 12, aliyeitwa Pacha, hakuwa pamoja nao Yesu alipokuja. **25** Basi wale wanafunzi wengine walikuwa wakimwambia: “Tumemwona Bwana!” Lakini akawaambia: “Nisipoona alama za misumari kwenye mikono yake na kutia kidole changu katika alama hizo kisha niutie mkono wangu ubavuni mwake,^b sitaamini kamwe.”

26 Basi, siku nane baadaye wanafunzi wake walikuwa tena ndani ya nyumba, na Tomasi alikuwa pamoja nao. Yesu akaja, ingawa milango ilikuwa imefungwa, naye akasimama katikati yao na kusema: “Na muwe na amani.”^c **27** Kisha akamwambia Tomasi: “Weka kidole chako hapa, uone mikono yangu, na ulete mkono wako uguse ubavu wangu, ili uache kuwa na shaka* bali uamini.” **28** Tomasi akamjibu: “Bwana wangu na Mungu wangu!” **29** Yesu akamwambia: “Je, umeamini kwa sababu umeniona? Wenye furaha ni wale ambao wanaamini ingawa bado hawajaona.”

30 Kwa kweli, Yesu alifanya pia miujiza mingine mingi mbele ya wanafunzi, ambayo haijaandikwa katika kitabu hiki cha kukunjwa.^d **31** Lakini mambo haya yameandikwa ili mwamini kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu, na kwa sababu ya kuamini, mpate uzima kupitia jina lake.^e

20:27 *Tnn., “kuwa asiyeamini.”

21 Baada ya mambo hayo, Yesu alijifunua* tena kwa wanafunzi kwenye Bahari ya Tiberia. Alijifunua katika njia hii. **2** Simoni Petro, Tomasi (aliyeitwa Pacha),^a Nathanaeli^b kutoka Kana ya Galilaya, wana wa Zebedayo,^c na wanafunzi wake wengine wawili, walikuwa pamoja. **3** Simoni Petro akawaambia: "Ninaenda kuvua samaki." Wakamwambia: "Sisi pia tutaenda nawe." Basi wakaenda, wakapanda mashua, lakini usiku huo hawakuvua chochote.^d

4 Hata hivyo, kulipoanza kupambazuka, Yesu alisimama kando ya bahari, lakini wanafunzi hawakutambua ni Yesu.^e **5** Basi Yesu akawauliza: "Watoto, mna chakula chochote?"* Wakamjibu: "Hapana!" **6** Akawaambia: "Utupeni wavu upande wa kulia wa mashua, nanyi mtapata." Basi wakautupa, lakini wakashindwa kuvuta kwa sababu samaki walikuwa wengi sana.^f **7** Ndiyo mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda^g akamwambia Petro: "Ni Bwana!" Simoni Petro, aliposikia kwamba ni Bwana, akavaa* vazi lake la nje kwa maana alikuwa uchi,^h akajitumbukiza baharini. **8** Lakini wale wanafunzi wengine wakaja katika ile mashua ndogo, wakiukokota wavu wenye samaki wengi kwa maana hawakuwa mbali na nchi kavu, walikuwa umbali wa mita 90* hivi.

9 Walipofika ufuoni wakaona moto wa makaa na

21:1 *Au "aliwatokea." 21:5 *Au "samaki wowote." 21:7 *Au "akajifunga."
^aAu "alikuwa amevaa mavazi machache." 21:8 *Karibu futi 300. Tnn., "mikono 200 hivi." Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 21

a Yoh 11:16
Yoh 20:24

b Yoh 1:45

c Mt 4:21

d Lu 5:4, 5

e Lu 24:15, 16
Yoh 20:11, 14

f Lu 5:4, 6

g Yoh 13:23
Yoh 19:26
Yoh 20:2

Safu ya 2

a Yoh 20:19, 26

b Lu 22:32
Mdo 20:28
1Pe 5:2, 3

c Mdo 1:15
Ebr 13:20
1Pe 2:25

d Yoh 10:14, 15

juu yake palikuwa na samaki na mkate. **10** Yesu akawaambia: "Leteni baadhi ya samaki mliowavua sasa hivi." **11** Basi Simoni Petro akapanda kwenye mashua na kuvuta hadi ufuoni wavu uliojaa samaki wakubwa 153. Inga-wa walikuwa wengi sana wavu haukupasuka. **12** Yesu akawaambia: "Njoooni mpate kiamshakinywa." Hakuna hata mmoja wa wanafunzi aliyekuwana na ujasiri wa kumuuliza: "Wewe ni nani?" kwa sababu walijua ni Bwana. **13** Yesu akaja, akachukua mkate na kuwapa, na samaki vilevile. **14** Sasa hiyo ilikuwa mara ya tatu^a Yesu kuwatokea wanafunzi baada ya kufufuliwa kutoka kwa wafu.

15 Baada ya kupata kiamshakinywa, Yesu akamuuliza Simoni Petro: "Simoni mwana wa Yohana, je, unanipenda kuliko hawa?" Petro akamjibu: "Ndiyo, Bwana, unajua ninakupenda." Yesu akamwambia: "Lisha wanakondoo wangu."^b **16** Akamuuliza mara ya pili: "Simoni mwana wa Yohana, je, unanipenda?" Petro akamjibu: "Ndiyo, Bwana, unajua ninakupenda." Yesu akamwambia: "Chunga kondoo wangu wadogo."^c **17** Akamuuliza mara ya tatu: "Simoni mwana wa Yohana, je, unanipenda?" Petro akahuzunika kwamba alimuuliza mara ya tatu: "Je, unanipenda?" Kwa hiyo akamjibu: "Bwana, wewe unajua mambo yote; unajua kwamba ninakupenda." Yesu akamwambia: "Lisha kondoo wangu wadogo."^d **18** Kwa kweli ninakuambia, ulipokuwa kijana, ulikuwa unavaa mwenye-

we na kutembea kokote uli-kotaka. Lakini utakapozee-ka, utanyoosha mikono yako na mtu mwingine atakuvali-sha na kukupeleka usikotaka.” **19** Alisema hivyo ili kuonye-sha angemtukuza Mungu kwa kifo cha namna gani. Baada ya kusema hayo, akamwambia: “Endelea kunifuata.”^a

20 Petro alipogeuka, akamwona mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda^b akiwafuata, yule ambaye kwenye mlo wa jioni alikuwa amee-gemea nyuma kifuani pa Yesu, akamuuliza: “Bwana, ni nani anayekusaliti?” **21** Basi alipomwona, Petro akamuuliza Yesu: “Bwana, namna gani kuhusu mtu huyu?” **22** Yesu akamwambia: “Ikiwa ni mape-nzi yangu akae mpaka nije,

SURA YA 21

a Mt 19:28
Yoh 12:26
Ufu 14:4

b Yoh 13:23
Yoh 20:2

Safu ya 2

a Yoh 13:23
Yoh 19:26
Yoh 20:2
Yoh 21:7

b Yoh 20:30, 31

hilo linakuhusuje? Wewe ende-lea kunifuata.” **23** Basi haba-ri ikaenea miongoni mwa aki-na ndugu kwamba mwanafun-zi huyo hatakufa. Hata hivyo, Yesu hakumwambia kwamba hatakufa, bali alisema: “Ikiwa ni mapenzi yangu akae mpaka nije, hilo linakuhusuje?”

24 Huyu ndiye mwanafun-zi^a anayetoa ushahidi huu kuhusu mambo haya, na ambaye aliyaandika mambo haya, nasi tunajua kwamba ushahidi wake ni wa kweli.

25 Kwa kweli, pia kuna mambo mengine mengi aliyo-fanya Yesu, ambayo kama ya-ngeandikwa kirefu, nadhani ulimwengu haungekuwa na nafasi ya kuviweka vita-bu vya kukunjwa ambavyo vi-ngeandikwa.^b

MATENDO YA MITUME

YALIYOMO

- Ujumbe kwa Theofilo (1-5)
Mashahidi mpaka sehemu ya mbali ya dunia (6-8)
Yesu apaa mbinguni (9-11)
Wanafunzi wakusanyika kwa umoja (12-14)
Mathia achaguliwa kuchukua mahali pa Yuda (15-26)
- Wanafunzi wapokea roho takatifu siku ya Pentekoste (1-13)
Hotuba ya Petro (14-36)
Umati wakubaliana na hotuba ya Petro (37-41)
Watu 3,000 wabatizwa (41)
Ushirika wa Kikristo (42-47)
- Petro amponya kilema aliyekuwa akiombaomba (1-10)

- Hotuba ya Petro kwenye Safu ya Nguzo za Sulemani (11-26)
“Kurudishwa kwa mambo yote” (21)
Nabii kama Musa (22)
- Petro na Yohana wakamatwa (1-4)
Idadi ya waamini yafikia wanaume 5,000 (4)
Kesi mbele ya Sanhedrini (5-22)
“Hatuwezi kuacha kusema” (20)
Wasali ili wapate ujasiri (23-31)
Wanafunzi washiriki vitu vyao pamoja (32-37)
 - Anania na Safira (1-11)
Mitume wafanya ishara nyingi (12-16)
Wafungwa gerezani, kisha waachiliwa huru (17-21a)
Washtakiwa mbele ya Sanhedrini tena (21b-32)

- 'Kumtii Mungu badala ya wanadamu' (29)
Ushauri wa Gamalieli (33-40)
Kuhubiri nyumba kwa nyumba (41, 42)
- 6 Wanaume saba wachaguliwa kuhudumu (1-7)
Stefano ashtakiwa kwamba amekufuru (8-15)
- 7 Hotuba ya Stefano mbele ya Sanhedrini (1-53)
Nyakati za wazee wa ukoo (2-16)
Uongozi wa Musa; Waisraeli waabudu sanamu (17-43)
Mungu haishi kwenye mahekalu yaliyojengwa na wanadamu (44-50)
Stefano apigwa mawe (54-60)
- 8 Sauli mtesaji (1-3)
Filipo apata matokeo mazuri katika huduma huko Samaria (4-13)
Petro na Yohana watumwa Samaria (14-17)
Simoni ajaribu kununua roho takatifu (18-25)
Toashi Mwethiopia (26-40)
- 9 Sauli akiwa njiani kuelekea Damasko (1-9)
Anania atumwa kumsaidia Sauli (10-19a)
Sauli ahubiri kumhusu Yesu huko Damasko (19b-25)
Sauli atembelea Yerusalemu (26-31)
Petro amponya Ainea (32-35)
Dorkasi mkarimu afufuliwa (36-43)
- 10 Maono ya Kornelio (1-8)
Maono ya Petro kuhusu wanyama waliotakaswa (9-16)
Petro amtembelea Kornelio (17-33)
Petro awatangazia habari njema watu wa mataifa (34-43)
"Mungu hana ubaguzi" (34, 35)
Watu wa mataifa wapokea roho takatifu na kubatizwa (44-48)
- 11 Petro atoa ripoti kwa mitume (1-18)
Barnaba na Sauli huko Antiokia ya Siria (19-26)
Wanafunzi waanza kuitwa Wakristo (26)
Agabo atabiri kuhusu njaa (27-30)
- 12 Yakobo auawa; Petro afungwa gerezani (1-5)
- Petro awekwa huru kimuujiza (6-19)
Malaika ampiga Herode (20-25)
- 13 Barnaba na Sauli watumwa wakiwa wamishonari (1-3)
Huduma huko Kipro (4-12)
Hotuba ya Paulo huko Antiokia ya Pisidia (13-41)
Amri ya kinabii ya kuwageukia watu wa mataifa (42-52)
- 14 Ongezeko na upinzani huko Ikoniamu (1-7)
Wadhaniwa kuwa miungu huko Lистра (8-18)
Paulo aokoka kufa baada ya kupigwa mawe (19, 20)
Kuyaimarisha makutaniko (21-23)
Kurudi huko Antiokia ya Siria (24-28)
- 15 Bishano kuhusu tohara huko Antiokia (1, 2)
Suala lapeleka Yerusalemu (3-5)
Wazee na mitume wafanya mkutano (6-21)
Barua kutoka baraza linaloongoza (22-29)
Kujiepusha na damu (28, 29)
Makutaniko yatiwa moyo kupitia barua (30-35)
Paulo na Barnaba waachana (36-41)
- 16 Paulo amchagua Timotheo (1-5)
Maono kuhusu mwanamume Mmakedonia (6-10)
Lidia awa mwamini huko Filipi (11-15)
Paulo na Sila wafungwa gerezani (16-24)
Mlinzi wa jela na nyumba yake wabatizwa (25-34)
Paulo ataka ombi rasmi la msamaha (35-40)
- 17 Paulo na Sila huko Thesalonike (1-9)
Paulo na Sila huko Beroia (10-15)
Paulo huko Athene (16-22a)
Hotuba ya Paulo katika Areopago (22b-34)
- 18 Huduma ya Paulo huko Korintho (1-17)
Kurudi Antiokia ya Siria (18-22)
Paulo aenda Galatia na Frigia (23)
Apolo mwenye ufasaha asaidiwa (24-28)
- 19 Paulo huko Efeso; baadhi ya watu wabatizwa tena (1-7)

- Paulo ajishughulisha na kazi ya kufundisha (8-10)
Mafanikio licha ya roho waovu (11-20)
Machafuko huko Efeso (21-41)
- 20 Paulo akiwa Makedonia na Ugiriki (1-6)
Eutiko afufuliwa huko Troa (7-12)
Kutoka Troa kwenda Mileto (13-16)
Paulo akutana na wazee wa Efeso (17-38)
Kufundisha nyumba kwa nyumba (20)
“Kuna furaha zaidi katika kutoa” (35)
- 21 Safarini kwenda Yerusalemu (1-14)
Kuwasili Yerusalemu (15-19)
Paulo afuata ushauri wa wazee (20-26)
Vurugu hekaluni; Paulo akamatwa (27-36)
Paulo aruhusiwa kuhutubia umati (37-40)
- 22 Paulo ajitetea mbele ya umati (1-21)
Paulo atumia uraia wake wa Roma (22-29)
Baraza la Sanhedrini lakutana (30)
- 23 Paulo azungumza mbele ya Sanhedrini (1-10)
Bwana amtia nguvu Paulo (11)
- Njama ya kumuua Paulo (12-22)
Paulo apeleka Kaisaria (23-35)
- 24 Mashtaka dhidi ya Paulo (1-9)
Paulo ajitetea mbele ya Feliksi (10-21)
Kesi ya Paulo yacheleweshwa kwa miaka miwili (22-27)
- 25 Kesi ya Paulo mbele ya Festo (1-12)
“Ninakata rufaa kwa Kaisari!” (11)
Festo ashauriana na Mfalme Agripa (13-22)
Paulo mbele ya Agripa (23-27)
- 26 Paulo ajitetea mbele ya Agripa (1-11)
Paulo aeleza jinsi alivyogeuka (12-23)
Maoni ya Festo na Agripa (24-32)
- 27 Paulo asafiri baharini kwenda Roma (1-12)
Meli yapigwa na dhoruba (13-38)
Wavunjikiwa na meli (39-44)
- 28 Ufuoni huko Malta (1-6)
Baba ya Publio aponywa (7-10)
Kuelekea Roma (11-16)
Paulo azungumza na Wayahudi huko Roma (17-29)
Paulo ahubiri kwa ujasiri kwa miaka miwili (30, 31)

1 Lile simulizi la kwanza, ewe Theofilo, niliandika kuhusu mambo yote ambayo Yesu alianza kufanya na kufundisha.^a **2** mpaka siku aliyochukuliwa kwenda juu,^b baada ya kuwapa mitume aliowachagua maagizo kupitia roho takatifu.^c **3** Baada ya kuteseka, alijionyesha kwao akiwa hai kupitia uthibitisho mwingi wenye kusadikisha.^d Wali mwona kwa siku 40, naye alizungumza nao kuhusu Ufalme wa Mungu.^e **4** Alipokuwa akikutana nao aliwaagiza hivi: “Msiondoke Yerusalemu,^f bali endeeleni kusubiri kile ambacho Baba ameahidi,^g ambacho mlinisikia nikisema kuhusu; **5** kwa maana Yohana,

SURA YA 1

- a Lu 1:3
Lu 3:23
b 1Ti 3:16
c Yoh 15:16
d Mt 28:9
Yoh 20:19
1Ko 15:4-7
e Lu 24:27
f Lu 24:49
g Yoh 14:16,17
Mdo 2:33

Safu ya 2

- a Yoe 2:28
Mt 3:11
Mk 1:8
b Lu 19:11
Lu 24:21
c Da 2:20, 21
Mt 24:36
d Mdo 4:33
e Isa 43:10
Lu 24:48
Yoh 15:26, 27
f Mdo 5:27, 28
g Mdo 8:14
h Kol 1:23

kwa kweli, alibatiza kwa maji, lakini ninyi mtabatizwa kwa roho takatifu^a baada ya siku chache.”

6 Basi, walipokusanyika, wakamuuliza: “Bwana, je, unaurudisha ufalme kwa Israeli wakati huu?”^b **7** Akawaambia: “Si juu yenu kujua nyakati au majira ambayo Baba ameweka katika mamlaka yake mwenyewe.^c **8** Lakini roho takatifu itakapokuja juu yenu mtapokea nguvu,^d nanyi mtakuwa mashahidi^e wangu katika Yerusalemu,^f katika Yudea yote na Samaria,^g na mpaka sehemu ya mbali zaidi* ya dunia.”^h **9** Baada ya kusema

1:8 *Au “miisho.”

mambo hayo, wakiwa wanatazama, akainuliwa juu na wingu likamfunika nao hawaku mwona tena.^a **10** Nao walipokuwa wakitazama angani akiwa anaenda, ghafla wanaume wawili wenye mavazi meupe^b wakasimama kando yao **11** na kusema: “Wanaume wa Galilaya, kwa nini mnasimama mkitazama angani? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenye mwendo angani atakuja vivyo hivyo kama vile ambavyo mmemwona akienda angani.”

12 Kisha wakarudi Yerusalem^c kutoka kwenye Mlima wa Mizeituni, ulio karibu na Yerusalemu, umbali wa safari ya siku ya sabato. **13** Walipofika, walienda kwenye chumba cha juu, walipokuwa wakikaa. Walikuwa Petro, Yohana, Yakobo, Andrea, Filippo, Tomasi, Bartholomayo, Mathayo, Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni mwenye bidii, na Yuda mwana wa Yakobo.^d **14** Wote hawa walidumu katika sala kwa kusudi moja, wakiwa pamoja na wanawake^e fulani na Maria mama ya Yesu, pamoja na ndugu za Yesu.^f

15 Katika siku hizo Petro akasimama kati ya akina ndugu (kwa ujumla idadi ya* watu ilikuwa karibu 120) na kusema: **16** “Wanaume, aki-na ndugu, ilikuwa lazima andiko litimizwe, ambalo roho takatifu ilisema kinabii kupitia Daudi kumhusu Yuda,^g aliye-waongoza wale waliomkamata Yesu.^h **17** Kwa maana alihesabiwa miongoni mwetuⁱ naye alipata fungu katika huduma hii. **18** (Mtu huyo ali-

1:15 *Au “umati wa.”

SURA YA 1

a Lu 24:51
Yoh 6:62

b Mt 28:2, 3

c Lu 24:52

d Mt 10:2-4
Mk 3:16-19

e Lu 23:49

f Mt 13:55
Yoh 7:5
Gal 1:19

g Zb 41:9
Zb 55:12
Yoh 13:18

h Lu 22:47
Yoh 18:3

i Mt 10:2, 4
Lu 6:12-16
Yoh 6:70, 71

Safu ya 2

a Zek 11:12
Mt 26:14, 15

b Mt 27:5-8

c Zb 69:25

d Zb 109:8

e Mt 3:13

f Lu 24:51
Mdo 1:9

g Mt 28:5, 6
Mk 16:6

h 1Sa 16:7
1Nya 28:9
Yer 11:20

i Yoh 6:70

j Met 16:33

nunua shamba kwa mshahara wa ukosefu wa uadilifu,^a akaanguka kichwa kwanzza, mwili wake ukapasuka* na matumbo yake yote yakamwagika.^b **19** Wakaaji wote wa Yerusalem wakajua jambo hilo, hivi kwamba shamba hilo likaitwa kwa lugha yao *Akeldama*, yaani, “Shamba la Damu.”) **20** Kwa maana imeandikwa katika kitabu cha Zaburi, ‘Makao yake yabaki kiwa, na pasiwe na mkaaji yeyote humo,’^c na, ‘Mtu mwingine na achukue cheo chake cha uangalizi.’^d **21** Kwa hiyo inafaa kwamba mmoja wa wanaume walioandamana nasi wakati wote ambao Bwana Yesu alifanya kazi zake* miongoni mwetu, **22** kuanzia alipobatizwa na Yohana^e mpaka siku alipochukuliwa kutoka kwetu kwenda juu,^f mmoja wa wanaume hao anapaswa kuwa shahidi pamoja nasi kuhusu ufufuo wake.”^g

23 Kwa hiyo wakapendekeza watu wawili, Yosefu aliyetiwa pia Barsaba au Yusto, na Mathia. **24** Ndipo wakasali wakisema: “Wewe, Ee Yehova,^{*} unayejuua mioyo ya wote,^h onyesha ni nani kati ya watu hawa wawili ambaye ume-mchagua **25** achukue mahali pa huduma na utume huu, ambao Yuda aliua na kwenda mahali pake mwenyewe.”ⁱ **26** Basi wakawapigia kura,^j na kura ikamwangukia Mathia, naye akahesabiwa* pamoja na wale mitume 11.

1:18 *Au “akapasuka katikati.” 1:21 *Au, “alipoingia na kutoka.” 1:24 *Angalia Nyongeza A5. 1:26 *Au “akajumlishwa,” yaani, akaonwa sawa na wale wengine 11.

2 Basi siku ya Sherehe ya Pentekoste^a ilipokuwa ikiendelea, wote walikuwa pamoja mahali palepale. **2** Ghafila kukatokea kelele kutoka mbinguni, kama ya upepo wenye nguvu unaovuuma, nao ukaijaza nyumba yote ambamo walikuwa wameketi.^b **3** Nao wakaona ndimi kama za moto, nazo zikagawanyika, na mmoja ukatua juu ya kila mmoja wao, **4** wote wakajazwa roho takatifu,^c wakaanza kusema katika lugha* mbalimbali, kama roho ilivyowawezesha kusema.^d

5 Wakati huo Wayahudi waliomwogopa Mungu kutoka kila taifa lililo chini ya mbingu walikuwa wakikaa Yerusalemu.^e **6** Basi sauti hiyo ilipotokea, umati ukakusanyika na kustaajabu, kwa sababu kila mmoja wao aliwasikia wakiongea katika lugha yake mwenyewe. **7** Kwa kweli, walishangaa sana na kusema: "Tazama, hawa wote wanaoongea ni Wagalilaya,^f sivyo? **8** Inakuwaje kwamba kila mmoja wetu anasikia lugha yake ya asili?" **9** Waparathi, Wamedi,^g na Waelami,^h wakaaaji wa Mesopotamia, Yudea na Kapadokia, Ponto na mkoa wa Asia,ⁱ **10** Frigia, Pamfilia, Misri, na maeneo ya Libya karibu na Kirene, wakaaaji wa muda wa kutoka Roma, Wayahudi na pia wageuzwa imani,^j **11** Wakrete, na Waarabu—tunawasikia wakisema katika lugha zetu kuhusu mambo makuu ya Mungu." **12** Ndiyo, wote wakashangaa na kustaajabu, wakauliza-

2:4 *Au "ndimi." 2:8 *Au "lugha yake ya kuzaliwa."

SURA YA 2

a Law 23:16
Kum 16:9-11

b Mdo 4:31

c Mk 1:8
Yoh 14:26

d Mdo 10:45, 46
1Ko 12:8, 10

e Kut 23:17

f Mk 14:70
Mdo 1:11

g 2Fa 17:6

h Da 8:1, 2

i 1Pe 1:1

j Kut 12:48

Safu ya 2

a Mdo 1:13

b Yoe 2:28

c 1Ko 12:8, 10

d Yoe 2:28-32
Ro 10:13

na: "Jambo hili linamaanisha nini?" **13** Hata hivyo, wengine wakawadhihaki na kusema: "Wamejaa divai tamu."*

14 Lakini Petro akasimama pamoja na wale 11^a na kuzungumza nao kwa sauti kubwa akisema: "Watu wa Yudea nanyi nyote wakaaji wa Yerusalemu, jueni jambo hili nanyi msikilize kwa makini maneno yangu. **15** Kwa kweli, watu hawa hawajalewa kama mnavyodhani, kwa maana ni saa tatu asubuhi. **16** Badala yake, hili ndilo lililosemwa kupitia nabii Yoeli: **17** "Na katika siku za mwisho," Mungu asema, "Nitaimimina sehemu ya roho yangu juu ya kila aina ya mwili, na wana wenu na mabinti wenu watatoa unabii, nao wanaume wenu vijana wataona maono, na wanaume wenu wazee wataota ndoto,^b **18** na hata juu ya watumwa wangu wa kiume na watumwa wa kike nitaimimina sehemu ya roho yangu siku hizo, nao watatoa unabii.^c **19** Nami nitafanya mambo ya ajabu* juu mbinguni na ishara chini duniani—damu na moto na mawingu ya moshi. **20** Jua litatiwa giza na mwezi utatiwa damu kabla ya kuja kwa ile siku ya Yehova* iliyo kuu na yenye utukufu. **21** Na kila mtu anayeliitia jina la Yehova* ataokolewa."^d

22 "Watu wa Israeli, sikieni maneno haya: Yesu Mnazareti alikuwa mwanamume ambaye Mungu alimwonyesha hadharani kwenu kupitia matendo

2:13 *Au "divai mpya." 2:19 *Au "miujiza." 2:20, 21 *Angalia Nyongeza A5.

yenye nguvu na mambo ya ajabu* na ishara ambazo Mungu alifanya kupitia kwake miongoni mwenu,^a kama mnavyoyua. **23** Mwanamume huyu, aliyekabidhiwa kupitia mapezi yaliyoamuliwa* na ujuzi wa awali wa Mungu,^b mlimfunga kwenye mti kupitia mkono wa waasi sheria, nanyi mkamua.^c **24** Lakini Mungu alimfufua^d kwa kumfungua kutoka katika maumivu makali ya* kifo, kwa sababu haingewezekana kifo kiendelee kumshika.^e **25** Kwa kuwa Daudi anasema hivi kumhusu: 'Nimemweka Yehova* mbele yangu^f daima, kwa maana yuko mkono wangu wa kulia ili nisitikiswe kamwe. **26** Kwa hiyo moyo wangu ulichangamka na ulimi wangu ukashangilia sana. Nami nitaisi* katika tumaini; **27** kwa sababu hutaniacha* Kaburini,^g wala hutamruhusu mshikamanifu wako aone uharibifu.^h **28** Umenijulisha njia za uzima; utanijaza shangwe nyingi mbele zako.*^g

29 "Wanaume, akina ndugu, inaruhusika nizungumze nanyi kwa uhuru wa kusema kumhusu Daudi kichwa cha familia, kwamba alikuwa, akazikwa,^h na kaburi lake liko hapaa kwetu mpaka leo. **30** Kwa sababu alikuwa nabii na alijua kwamba Mungu ali-

2:22 *Au "miujiza." 2:23 *Au "shauri lililoamuliwa." 2:24 *Au labda, "kamba za." 2:25, 34, 39 *Angalia Nyongeza A5. 2:25 #Au "mbele ya macho yangu." 2:26 *Tnn., "mwili wangu utaisi." 2:27 *Au "hutaiacha nafsi yangu." 2:27, 31 #Au "Hadesi." Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:27 ^hAu "hutaruhusu mwili wake uoze." 2:28 *Au "mbele za uso wako."

SURA YA 2

a Yoh 5:36
Yoh 14:10

b Yoh 19:10, 11
Mdo 4:27, 28
1Pe 1:20

c Lu 23:33
Mdo 5:30
Mdo 7:52

d Mdo 3:15
Ro 4:24
1Ko 6:14
Kol 2:12
Ebr 13:20

e Yoh 10:17, 18

f Mdo 13:35

g Zb 16:8-11

h 1Fa 2:10

Safu ya 2

a 2Sa 7:12, 13
Zb 89:3, 4
Zb 132:11

b Zb 16:10

c Lu 24:46-48
Mdo 1:8
Mdo 3:15

d Ro 8:34
Flp 2:9-11
1Pe 3:22

e Yoh 14:26

f Zb 110:1
Lu 20:42, 43
1Ko 15:25
Ebr 10:12, 13

g Mt 28:18
Yoh 3:35
Mdo 5:31

h Yoh 19:6

i Lu 24:46, 47
Mdo 17:30
Mdo 26:20

j Mt 28:19

k Mt 26:27, 28
Efe 1:7

l Yoe 2:28

kuwa amemwambia kwa kiapo kwamba angemfanya mmoja wa wazao wake* aketi kwenye kiti chake cha ufalme,^a **31** aliona mapema na kusema kuhusu ufufu wa Kristo, kwamba hakuachwa katika Kaburi^h wala mwili wake haukuona uharibifu.*^b **32** Mungu alimfufua, Yesu huyu, na sisi sote ni mashahidi wa jambo hilo.^c **33** Kwa hiyo, kwa sababu aliinuliwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu^d na kupokea roho takatifu iliyoahidiwa kutoka kwa Baba,^e amemimina hiki mnachoona na kusikia. **34** Kwa kuwa Daudi hakupanda mbinguni, bali yeye mwenyewe anasema, 'Yehova* alimwambia Bwana wangu: "Keti kwenye mkono wangu wa kuume **35** mpaka niwaweke maadi wako kuwa kiti cha miguu yako."^f **36** Kwa hiyo, nyumba yote ya Israeli na ijue kwa hakika kwamba Mungu alimfanya Bwana^g na pia Kristo, Yesu huyu ambaye ninyi mlimuua kwenye mti."^h

37 Basi waliposikia hilo, walichomwa moyoni, nao wakamwambia Petro na wale mitume wengine: "Wanaume, akina ndugu, tufanye nini?" **38** Petro akawaambia: "Tubuni,ⁱ na kila mmoja wenu abatizwe^j katika jina la Yesu Kristo ili msamehewe dhambi zenu,^k nanyi mtapokea zawadi ya bure ya roho takatifu. **39** Kwa maana ahadi^l hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa wale wote walio mbali, kwa wote ambao huenda Yehova* Mungu wetu

2:30 *Tnn., "mmoja kati ya wazao wa kiuno chake." 2:31 *Au "haukuoza."

akawaita kwake.”^a **40** Akae-ndealea kuwahimiza na kutoa ushahidi kamili kwa maneno mengine mengi, akisema: “Okoleweni kutoka katika kizazi hiki kilichopotoka.”^b

41 Basi wale waliokubali neno lake kwa furaha wakatibizwa,^c na siku hiyo karibu watu 3,000 wakaongezwa.*^d

42 Nao wakaendelea kujitoa kwa bidii kwa fundisho la mitume, kushirikiana pamoja,* kula milo,^e na kusali.^f

43 Kwa kweli, kila mtu akawa* na hofu, nao mitume wakaanza kufanya mambo mengi ya ajabu^g na ishara nyingi.^g

44 Wale wote ambao sasa walikuwa waamini walikusanyika pamoja na wakashirikiana katika mambo yote, **45** nao walikuwa wakiuza mali zao^h na vitu walivyomiliki na kuwagawia wote pesa walizopata, kulingana na uhitaji wa kila mtu.ⁱ **46** Kila siku walihudhuria daima kwenye hekalu kwa kusudi moja, nao walikula milo yao katika nyumba mbalimbali na kushiriki chakula chao kwa shangwe nyingi na kwa moyo mweupe, **47** wakimsifu Mungu na kupata kabali kwa watu wote. Wakati uleule Yehova* akae-ndealea kuwaongezea kila siku watu waliokuwa wakiokolewa.^j

3 Basi Petro na Yohana walikuwa wakipanda kwen-
da hekaluni wakati wa saa ya sala, yaani, saa tisa,* **2** na mwanamume fulani aliyek-
wa kilema tangu kuzaliwa ali-

2:41 *Au “nafsi 3,000 zikaongezeka.”

2:42 *Au “kushiriki vitu na wengine.”

2:43 *Au “kila nafsi ikawa.” *Au “miujiza mingi.” 2:47 *Angalia Nyongeza A5. 3:1 *Yaani, karibu saa 9 alasiri.

SURA YA 2

a Yoe 2:32

b Kum 32:5
Zb 78:8

c Mdo 8:12
Mdo 18:8

d Mdo 4:4
Mdo 5:14

e Mdo 2:46

f Mdo 1:14

g Mdo 5:12

h Mt 19:21

i Mdo 4:32, 34

j Mdo 5:14
Mdo 11:21
Iko 3:7

Safu ya 2

SURA YA 3

a Mdo 3:16
Mdo 4:10

b Mt 8:14, 15
Mt 9:24, 25

c Yoh 5:8, 9
Mdo 9:34
Mdo 14:8-10

d Isa 35:6

e Mdo 3:2

f Yoh 10:23
Mdo 5:12

kuwa amebebwa. Kila siku walimweka karibu na lango la hekalu lililoitwa Lango Zuri, ili aombe zawadi za rehema kutoka kwa wale waliokuwa wakiingia hekaluni. **3** Alipo-waona Petro na Yohana wa-kiwa karibu kuingia hekalu-ni, akaanza kuomba zawadi za rehema. **4** Lakini Petro, pamoja na Yohana, wakamtazama moja kwa moja na kumwambia: “Tuan-galie.” **5** Kwa hiyo akawaan-galia, akitarajia kupata kitu kutoka kwao. **6** Hata hivyo, Petro akasema: “Sina fedha wala dhahabu, lakini kile nili-cho nacho ndicho ninachoku-pa. Katika jina la Yesu Kri-sto Mnazreti, tembea!”^a **7** Ndipo akamshika mkono wa kulia na kumwinua.^b Papo hapo miguu yake na vifundo vya miguu yake vikafanywa imara;^c **8** akasimama mara moja,^d akaanza kutembea na kuingia nao hekaluni, akitem-bea na kurukaruka akimsi-fu Mungu. **9** Watu wote wa-kamwona akitembea huku akimsifu Mungu. **10** Wakaa-nza kutambua kwamba huyu ndiye mtu aliyekuwa akiketi kwenye Lango Zuri la hekalu^e akisubiri zawadi za rehema, nao wakashangaa sana na ku-shangilia kuhusu jambo lililo-tokea.

11 Mtu huyo akiwa bado amewashika Petro na Yoha-na, watu wote wakawakimbi-lia pamoja kwenye sehemu ili-yoitwa Safu ya Nguzo za Sule-mani,^f wakiwa wameshangaa sana. **12** Petro alipoona jambo hilo, akawaambia watu hao: “Watu wa Israeli, kwa nini mnastaajabishwa na jambo hili, na kwa nini

mnatutazama kana kwamba tumemfanya atembea kwa nguvu zetu au kwa sababu ya ujitoaji-kimungu?* **13** Mungu wa Abrahamu na wa Isaka na wa Yakobo,^a Mungu wa mababu zetu, amemtukuza Mtumishi wake,^b Yesu,^c ambaye ninyi mlimkabidhi^d na kumkana mbele ya Pilato, ingawa alikuwa ameamua kumfungua. **14** Ndiyo, mlimkana huyo aliyetakatifu na mwadilifu, nanyi mkaomba mpewe mwanaumume aliyekuwa muuaji,^e **15** lakini mkamuua Wakili Mkuu wa uzima.^f Hata hivyo, Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, nasi ni mashahidi wa jambo hilo.^g **16** Kupitia jina lake, na kwa imani yetu katika jina lake, mtu huyu mnayemwona na kumfahamu amefanywa awe mwenye nguvu. Imani kupitia kwake imemfanya mtu huyu awe mwenye afya kamili, mbele yenu nyote. **17** Na sasa, akina ndugu, ninajua kwamba mlitenda kwa kutojua,^h kama vile watawala wenu pia walivyotenda.ⁱ **18** Lakini kwa njia hiyo Mungu ametimiza mambo aliyotangaza mapema kupitia kinywa cha manabii wote, kwamba Kristo wake angeteseka.^j **19** "Kwa hiyo, tubuni^k na mgeuke^l ili dhambi zenu zifutwe,^m ili majira yenye kuburudisha yaje kutoka kwa Yehova mwenyewe,* **20** naye amtume Kristo aliyewekwa rasmi kwa ajili yenu, yaani, Yesu. **21** Naye lazima abaki mbinguni mpaka nyakati za kurudishwa kwa mambo yote

3:12 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 3:19 *Tnn., "kutoka kwa uso wa Yehova." Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 3

- a Kut 3:6
b Isa 52:13
Isa 53:11
c Flp 2:9-11
d Mdo 5:30
e Mt 27:20, 21
Lu 23:14, 18
f Mdo 5:31
Ebr 2:10
g Lu 24:46-48
Mdo 1:8
Mdo 2:32
h Yoh 16:2, 3
1Ti 1:13
i 1Ko 2:8
j Zb 118:22
Isa 50:6
Isa 53:8
Da 9:26
Lu 22:15
k Mdo 2:38
l Eze 33:11
Efe 4:22
m Eze 33:14, 16
1Yo 1:7

Safu ya 2

- a Kum 34:10
Mdo 7:37
b Kum 18:15, 18
c Kum 18:19
d Lu 24:27
Mdo 10:43
e Ro 9:4
f Mwa 22:18
Gal 3:8
g Mdo 13:45, 46
Ro 1:16

SURA YA 4

- h Mdo 23:8
i Mdo 4:33
Mdo 17:18
j Lu 21:12
k Mdo 2:41
Mdo 6:7

ambayo Mungu alisema kupitia kinywa cha manabii wake watakatifu walioishi zamani. **22** Kwa kweli, Musa alisema: "Yehova* Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka kati ya ndugu zenu.^a Ni lazima msikilize kile atakachowaambia.^b **23** Kwa kweli, yeyote* ambaye hatamsikiliza Nabii huyo ataangamizwa kutoka kati ya watu.^c **24** Manabii wote kuanzia Samweli na wale waliofuata, wengi ambao wamesema, wametangaza waziwazi pia kuhusu siku hizi.^d **25** Ninyi ndio wana wa manabii na wa agano ambalo Mungu alifanya na mababu zenu,^e alipomwambia Abrahamu: "Kupitia uzao wako,* familia zote za dunia zitabarikiwa."^f **26** Baada ya Mungu kumwinua Mtumishi wake, alimtuma kwenu kwanza^g ili awabariki ninyi kwa kumgeuzi kila mmoja wenu aache matendo yake maovu."

4 Hao wawili walipokuwa wakizungumza na watu, makuhani, kapteni wa hekalu, na Masadukayo^h wakawajia. **2** Walikuwa wameudhika kwa sababu mitume walikuwa wakiwafundisha watu na kutangaza waziwazi kwamba Yesu alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu.ⁱ **3** Basi wakawakamata na kuwaweka kizuzini^j mpaka siku iliyofuata, kwa maana tayari ilikuwa jioni. **4** Hata hivyo, wengi waliokuwa wamesikiliza maneno hayo wakaamini, na idadi ya wanaume ikawa karibu 5,000.^k

3:22 *Angalia Nyongeza A5. 3:23 *Au "nafsi yoyote." 3:25 *Tnn., "mbegu yako." 4:2 *Au "kufufuliwa kutoka kwa wafu katika kisa cha Yesu."

5 Siku iliyofuata watawala wao, wazee, na waandishi wakakusanyika pamoja huko Yerusalemu 6 pamoja na Anasi^a mkuu wa makuhani, Kayafa,^b Yohana, Aleksanda, na wote waliokuwa watu wa ukoo wa mkuu wa makuhani. 7 Wakawasimamisha Petro na Yohana katikati yao na kuanza kuwauliza: “Mlifanya jambo hilo kwa nguvu gani au katika jina la nani?” 8 Ndipo Petro, akiwa amejaa roho takatifu,^c akawaambia:

“Watawala wa watu na wazee, 9 ikiwa tunahojiwa leo kuhusu tendo jema alilofanyika mtu huyu aliyekuwa kilema,^d na ikiwa mnataka kujua aliyemponya, 10 na ijulikane kwenu nyote na kwa watu wote wa Israeli kwamba katika jina la Yesu Kristo Mnazareti,^e ambaye mlimuua kwenye mti^f lakini Mungu akamfuua kutoka kwa wafu,^g kupitia kwake mtu huyu anasimama hapa mbele yenu akiwa ameponywa. 11 Hilo ndilo ‘jiwe ambalo ninyi wajenzi mlilitendea kana kwamba halina maana nalo limekuwa jiwe kuu la pembeni.’^{*h} 12 Zaidi ya hayo, hakuna wokovu katika mwingine yeyote, kwa maana hakuna jina lingineⁱ chini ya mbingu walilopewa wadamu ambalo kupitia hilo tunaweza kuokolewa.”^j

13 Walipoona Petro na Yohana wakizungumza kwa ujasisiri, ingawa walikuwa watu wasio na elimu* na wa kawaida tu,^k wakashangaa. Nao wa-

4:11 *Tnn., “kichwa cha pembeni.”

4:13 *Yaani, hawakuwa na elimu ya shule za kirabi; haimaanishi hawakujua kusoma na kuandika.

SURA YA 4

a Yoh 18:13

b Mt 26:57
Lu 3:2
Yoh 11:49-51

c Mdo 7:55

d Mdo 3:7

e Mdo 3:6

f Mdo 2:36

g Mdo 2:24
Mdo 5:30h Zb 118:22
Isa 28:16
Mt 21:42
1Pe 2:7i Mt 1:21
Mdo 10:43
Flp 2:9,10j Yoh 1:12
Yoh 14:6
1Ti 2:5, 6k Mt 11:25
1Ko 1:26, 27

Safu ya 2

a Yoh 7:14, 15

b Mdo 3:11

c Lu 21:15

d Yoh 11:47

e Mdo 3:9, 10

f Mdo 5:40

g Mdo 5:29

h Lu 22:2
Mdo 5:26

katambua kwamba walikuwa pamoja na Yesu.^a 14 Walipokuwa wakimtazama yule mtu aliyekuwa ameponywa, akiwa amesimama pamoja nao,^b hawakuwa na jambo la kusema.^c 15 Basi wakawaamuru waende nje ya jumba la Sanhedrini, kisha wakaanza kushauriana, 16 wakisema: “Tufanye nini na watu hawa?^d Kwa sababu kwa kweli ishara kubwa imetukia kupitia kwao ambayo imejulikana na wakaaji wote wa Yerusalemu,^e nasi hatuwezi kuikana. 17 Ili jambo hili lisizidi kusambazwa kati ya watu, basi tuwatishe na kuwaambia wasizungumze tena na mtu yeyote kwa msingi wa jina hilo.”^f

18 Ndipo wakawaita na kuwaamuru wasiseme lolote wala kufundisha kwa msingi wa jina la Yesu. 19 Lakini Petro na Yohana wakawajibu: “Kama ni sawa machoni pa Mungu kuwasikiliza ninyi badala ya Mungu, hukumuni ninyi wenyewe. 20 Lakini sisi hatuwezi kuacha kusema kuhusu mambo ambayo tumeyaona na kuyasikia.”^g 21 Basi baada ya kuwatisha zaidi, wakawafungua, kwa vile hawakupata msingi wowote wa kuwadhibu na kwa kuwa waliwaogopa watu,^h kwani wote walikuwa wakimtukuza Mungu kwa sababu ya jambo lililokuwa limetukia. 22 Kwa maana yule mtu ambaye alifanyiwa muujiza huo* wa kuponywa alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 40.

23 Baada ya kufunguliwa, wakaenda kwa watu wao na kuwaeleza mambo

4:22 *Au “ishara hiyo.”

waliyoambiwa na wakuu wa makuhani na wazee. **24** Waliposikia hayo, wote kwa pamoja wakasali kwa Mungu wakisema kwa sauti kubwa:

“Bwana Mwenye Enzi Kuu, wewe Ndiye uliyeeumba mbingu, dunia, bahari, na vitu vyote vilivyomo,^a **25** nawe ulisema kupitia roho takatifu kwa kinywa cha babu yetu Daudi,^b mtumishi wako: ‘Kwa nini mataifa yalikuwa na msukosuko na watu wakatafakari mambo matupu? **26** Wafalme wa dunia walijipanga nao watawala wakakusanyika pamoja kama kitu kimoja dhidi ya Yehova* na dhidi ya mtiwamafuta wake.’^{#c} **27** Kwa kweli Herode na Pontio Pilato^d pamoja na watu wa mataifa na watu wa Israeli walikusanyika katika jiji hili dhidi ya mtumishi wako mtakatifu Yesu, ambaye ulimtia mafuta,^e **28** ili wafanye yale ambayo mkono na shauri lako liliazimia awali yatukie.^f **29** Na sasa, Yehova,* angalia vitisho vyao, nawe uwaweze she watumwa wako waendele kutangaza neno lako kwa ujasiri wote, **30** huku ukinyoosha mkono wako ili uponye, na huku ishara na mambo ya ajabu* yakitukia^g kupitia jina la mtumishi wako mtakatifu Yesu.”^h

31 Na baada ya kutoa dua,* mahali walipokuwa wamekusanyika pakatikiswa, na kila mmoja wao akajazwa roho takatifuⁱ nao walikuwa wakitangaza neno la Mungu kwa ujasiri.^j

4:26, 29 *Angalia Nyongeza A5. 4:26 #Au “Kristo wake.” 4:30 *Au “miujiza.” 4:31 *Au “waliposali kwa bidii.”

SURA YA 4

a Kut 20:11
Ne 9:6
Zb 146:6

b 2Sa 23:1, 2

c Zb 2:1, 2

d Lu 23:12

e Zb 45:7
Mdo 10:38

f Isa 53:10
Lu 24:44
Mdo 2:23
1Pe 1:20

g Mdo 2:43
Mdo 5:12

h Mdo 3:16

i Mdo 2:2, 4

j 1Th 2:2

Safu ya 2

a Mdo 2:44, 45

b Mdo 1:21, 22
Mdo 4:2

c Mdo 2:44, 45

d Mdo 5:1, 2

e Mdo 6:1

f Mdo 11:22
Mdo 12:25

g Lu 12:33

SURA YA 5

h Mdo 4:34, 35

i Zb 101:7
Efe 4:25
Kol 3:9

j Mdo 5:9

32 Isitoshe, umati uliokuwa umeamini ulikuwa na moyo na nafsi* moja, na hakuna hata mmoja wao aliyeona vitu vya-ke kuwa mali yake mwenyewe, bali walishiriki pamoja vitu vyote walivyokuwa navyo.^a **33** Na kwa nguvu nyingi, mitume wakaendelea kutoa ushahidi kuhusu ufufuo wa Bwana Yesu,^b na fadhili zisizostahiliwa zilikuwa pamoja nao kwa kadiri kubwa. **34** Kwa kweli, hakuna yeyote kati yao aliyekuwa na uhita-ji,^c kwa maana wote waliokuwa na mashamba au nyumba walikuwa wakiuza na kuleta thamani ya kile walichouza, **35** na kukiweka miguuni pa mitume.^d Kisha kila mmoja aligawiwa kulingana na uhita-ji wake.^e **36** Kwa hiyo Yosefu, ambaye pia mitume walimwita Barnaba^f (jina ambalo linapotafsiriwa linamaanisha, “Mwana wa Faraja”), Mlawi, mzaliwa wa Kipro, **37** alikuwa na shamba, akalizuza, akaleta pesa na kuziweka miguuni pa mitume.^g

5 Hata hivyo, mwanamume fulani aliyelitwa Anania, pamoja na Safira mke wake, waliuza mali. **2** Lakini akajiwekea kisiri kiasi fulani, mke wake pia akijua jambo hilo, naye akaleta sehemu fulani tu na kuiweka miguuni pa mitume.^h **3** Lakini Petro akamuu- liza: “Anania, kwa nini She- tani amekupa ujasiri wa kui- danganyaⁱ roho takatifu^j uka- jiwekea kisiri kiasi fulani cha bei ya shamba? **4** Kabla ya kuliuza, je, halikuwa mali yako? Na baada ya kuliuza, je, pesa hizo hazikuwa mikononi

4:32 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

mwako? Kwa nini umewaza tendo kama hili moyoni mwako? Umedanganya si wanadamu, bali Mungu.” **5** Anania aliposikia maneno hayo, akaanguka chini akafa. Na wote waliosikia jambo hilo wakaogopa sana. **6** Basi vijana wakasimama, wakamfunga kwa vitambaa, wakamtoa nje, na kumzika.

7 Sasa baada ya muda wa saa tatu hivi, mke wake akaingia bila kujua kilichokuwa kimetokea. **8** Petro akamuuliza: “Niambie, je, ninyi wawili mliuza shamba kwa kiasi hiki?” Akajibu: “Ndiyo, kwa kiasi hicho.” **9** Kwa hiyo Petro akamwambia: “Kwa nini ninyi wawili mlikubaliana kujaribu roho ya Yehova?” Tazama! Miguu ya wale waliomzika mume wako, ipo mlangoni, nao watakubeba na kukutoa nje.” **10** Papo hapo akaanguka chini miguuni pa Petro akafa. Wale vijana walioplingia walikuta amekufa, wakamtoa nje na kumzika kando ya mume wake. **11** Basi kutaniko lote na wote waliosikia kuhusu mambo hayo wakaogopa sana.

12 Isitoshe, kupitia mikono ya mitume ishara nyingi na mambo ya ajabu* yakaendelea kutukia kati ya watu;^a na wote walikuwa wakikutana kwenye Safu ya Nguzo za Sulemani.^b **13** Kwa kweli, hakuna yeyote kati ya wale wengine aliyekuwa na ujasiri wa kujiunga nao; hata hivyo, watu walikuwa wakiwasifu. **14** Isitoshe, wale waliomwamini Bwana wakazidi kuongezeka, ida-

5:9, 19 *Angalia Nyongeza A5. 5:12 *Au “miujiza.”

SURA YA 5

a Mdo 4:29, 30
Mdo 6:8
Mdo 14:3
Mdo 15:12
Ro 15:18, 19
2Ko 12:12

b Yoh 10:23
Mdo 3:11

Safu ya 2

a Mdo 6:7

b Mt 9:20, 21

c Lu 21:12

d Zb 34:7
Mdo 12:7
Mdo 16:26
Ebr 1:7, 14

di kubwa ya wanaume na wanawake.^a **15** Hata wakawaleta wagonjwa kwenye njia kuu na kuwalaza kwenye vitanda vidogo na mikeka, ili Petro akipita hapo, angalau kivuli chake kiwaangukie baadhi yao.^b **16** Pia, umati kutoka kwenye majiji yaliyokuwa karibu na Yerusalemu ukazidi kuja, ukiwa umewabeba wagonjwa na wale waliosumbuliwa na roho waovu, nao wote wakaponywa.

17 Lakini kuhani mkuu akasimama, na wote waliokuwa pamoja naye, ambao walikuwa wafuasi wa madhehebu ya Masadukayo, nao walikuwa wamejaa wivu. **18** Basi wakawakamata mitume na kuwafunga katika jela ya watu wote.^c **19** Lakini usiku, malaika wa Yehova* akaifungua milango ya gereza,^d akawatoa nje na kuwaambia: **20** “Nendeni mkasimame hekaluni, na mwendelee kuwaambia watu maneno yote kuhusu maisha haya.” **21** Baada ya kusikia hilo, wakaingia hekaluni wakati wa mapambazuko na kuanza kufundisha.

Basi kuhani mkuu na wale waliokuwa pamoja naye walipofika, wakakusanya Sanhedrini na kusanyiko lote la wazee wa wana wa Israeli, nao wakawatuma watu kwenye jela ili wawalete mitume mbele yao. **22** Lakini wale maofisa walipofika huko, hawakuwakuta gerezani. Basi wakarudi na kutoa taarifa, **23** wakisema: “Tuliikuta jela ikiwa imefungwa kabisa na wali-nzi wakiwa wamesimama kwenye milango, lakini tuli-poifungua hatukumkuta mtu

yeyote ndani.” **24** Basi, kapteni wa hekalu na wakuu wa makuhani waliposikia maneno hayo, walifadhaika sana kwa kuwa hawakujua jambo hilo lingekuwa na matokeo gani. **25** Lakini mtu fulani akaja na kuwaambia: “Tazameni! Wale watu mliowafunga gerezani wako hekaluni, wakiwa wamesimama wakifundisha watu.” **26** Ndi-po kapteni akaenda pamoja na maofisa wake na kuwaleta bila kutumia nguvu, kwa maana waliogopa watu watawapi-ga mawe.^a

27 Basi wakawaleta na kuwasimamisha mbele ya Sanhedrini. Kisha kuhani mkuu akawahoji **28** akisema: “Tuliwakataza kabisa msifundishe kwa msingi wa jina hili,^b na bado tazama! mmejaza Yerusalemu fundisho lenu, nanyi mmeazimia kuileta damu ya mtu huyu juu yetu.”^c **29** Petro na wale mitume wengine wakajibu: “Lazima tumtii Mungu kuwa mtawala bada-la ya wanadamu.^d **30** Mungu wa mababu zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimuua, kwa kumtundika kwenye mti.^e **31** Mungu alimwinua huyu kuwa Wakili Mkuu^f na Mwokozi^g kwenye mkono wake wa kuume,^h ili kuwapa Israeli toba na msamaha wa dhambi zao.ⁱ **32** Nasi ni mashahidi wa mambo hayo,^j na pia roho takatifu,^k ambayo Mungu amewapa wale wanaomtii aki-wa mtawala.”

33 Waliposikia hayo, waka-kasirika sana* nao wakata-ka kuwaangamiza. **34** Lakini Farisayo mmoja aitwaye Ga-

5:33 *Au “wakahisi wamechomwa.”

SURA YA 5

a Lu 20:19

b Mdo 4:18

c Mt 27:25
Mdo 3:14, 15d Da 3:17, 18
Mdo 4:19, 20

e Mdo 2:23, 24

f Mdo 3:15

g Mt 1:21
Ebr 2:10h Mdo 2:32, 33
Flp 2:9i Isa 53:11
Mdo 2:38
Mdo 10:43j Lu 24:46-48
Mdo 1:8

k Yoh 15:26

Safu ya 2

a Mdo 22:3

b Met 21:30

c Mdo 26:14

d Mt 10:17
Mk 13:9e Mt 5:12
Mdo 16:25
Ro 5:3
2Ko 12:10
Flp 1:29
Ebr 10:34
1Pe 4:13

f Mdo 20:20

g Mdo 4:31

malieli^a akasimama katika Sanhedrini; alikuwa mwali-mu wa Sheria aliyeheshimiwa na watu wote, naye akaamu-ru watu hao watolewe nje kwa muda mfupi. **35** Kisha aka-waambia: “Wanaume wa Israe-li, iweni waangalifu kuhusu jambo mnalokusudia kuwa-tendea watu hawa. **36** Kwa mfano, kabla ya siku hizi Theuda alisimama akidai kwa-mba yeye ni mtu wa maana, na wanaume kadhaa, karibu 400, wakajiunga na chama chake. Lakini aliangamizwa, na wa-fuasi wake wote wakatawa-nyika na kwisha. **37** Baada yake, Yuda Mgalilaya akainu-ka katika zile siku za uandiki-shaji, naye akawa na wafuasi. Mtu huyo pia aliangamia, na wafuasi wake wote wakatawa-nyika. **38** Basi chini ya hali zilizopo, ninawaambia, msi-ingilie mambo ya watu hawa, bali waacheni. Kwa maana, ikiwa mpango huu au kazi hii ni ya wanadamu, itaangami-za; **39** lakini ikiwa imetoka kwa Mungu, hamtaweza ku-waangamiza.^b La sivyo, hue-nda ikawa mnapigana na Mu-ngu mwenyewe.”^c **40** Ndipo wakasikiliza ushauri wake, wakawaita mitume, wakawapi-ga viboko,^d na kuwaagiza wa-ache kusema kwa msingi wa jina la Yesu, kisha wakawaa-cha waende.

41 Basi wakatoka mbele ya Sanhedrini, wakishangi-lia^e kwa sababu walikuwa wamestahili kuvunjiwa heshi-ma kwa ajili ya jina lake. **42** Na kila siku hekaluni na nyumba kwa nyumba^f wakae-ndelea kufundisha na kuta-ngaza habari njema kumhusu Kristo Yesu bila kuacha.^g

6 Basi katika siku hizo, wanafunzi walipokuwa wakiongezeka, Wayahudi waliozungumza Kigiriki walianza kulalamika kuhusu Wayahudi waliozungumza Kiebrania, kwa sababu wajane wao walikuwa wakipuuzwa katika ugawaji wa kila siku.^a **2** Basi wale 12 wakauita umati wa wanafunzi na kuwaambia: “Si vema* sisi tuache neno la Mungu ili kugawa chakula mezani.^b **3** Basi akina ndugu, jichagulieni kati yenu wanau-me saba wenye sifa nzuri,^c waliojaa roho na hekima,^d ili tuwaweke rasmi wafanye kazi hii muhimu;^e **4** lakini sisi tutajitoa kwa sala na huduma ya neno.” **5** Wanafunzi wote wakakubaliana na jambo walilosema, nao wakamchagua Stefano, mwanamume aliyejaa imani na roho takatifu, vilevile Filippo,^f Prokoro, Nikanori, Timoni, Parmena, na Nikolao, mgeuzwa-imani wa Antiokia. **6** Wakawaleta kwa mitume, na baada ya kusali, wakaweka mikono juu yao.^g

7 Kwa hiyo, neno la Mungu likazidi kuenea,^h na idadi ya wanafunzi ikazidi kuongezeka sanaⁱ huko Yerusalemu; na umati mkubwa wa makuhani wakawa waamini.^j

8 Sasa Stefano, akiwa amejaa kibali cha Mungu na nguvu, alikuwa akifanya mambo makubwa ya ajabu* na ishara kati ya watu. **9** Lakini watu fulani wa Sinagogi la Watu Waliowekwa Huru wakaja mbele, pamoja na Wakirene na Waaleksandria, na wengine kutoka Kilikia na Asia, ili ku-

6:2 *Tnn., “Haipendezi.” 6:8 *Au “miujiza.”

SURA YA 6

a Mdo 4:34, 35
ITI 5:3
Yak 1:27

b Kut 18:17, 18

c Mdo 16:1, 2
ITI 3:7

d Mdo 6:8, 10

e Kum 1:13

f Mdo 21:8

g Kum 34:9
Mdo 8:14, 17
Mdo 13:2, 3
ITI 4:14
ITI 5:22
ZTI 1:6

h Mdo 12:24
Mdo 19:20

i Mdo 2:47

j Yoh 12:42
Mdo 15:5

Safu ya 2

a Isa 54:17
Lu 21:15
Mdo 6:3

SURA YA 7

b Mwa 11:31

c Mwa 12:1

d Mwa 11:32

e Mwa 12:4, 5
Ebr 11:8

bishana na Stefano. **10** Lakini hawakuweza kumshinda kwa sababu ya hekima yake na roho iliyomwongoza kusema.^a **11** Ndipo wakawashawishi watu kwa siri waseme: “Tumemsikia akisema maneno ya kumkufuru Musa na Mungu.” **12** Nao wakawachocha watu, wazee, na waandishi, wakamjia ghafla, wakamkamata kwa nguvu na kumpeleka kwenye Sanhedrini. **13** Wakawaleta mbele mashahidi wa uwongo, waliosema: “Mtu huyu haachi kusema mambo yasiyofaa kuhusu mahali hapa patakatifu na kuhusu Sheria. **14** Kwa mfanano, tumemsikia akisema kwamba huyu Yesu Mnazareti atapaangusha mahali hapa na kuzibadili desturi ambazo Musa alitukabidhi.”

15 Wote waliokuwa wameketi katika Sanhedrini wakamkazia macho, nao wakaona uso wake ukiwa kama uso wa malaika.

7 Lakini kuhani mkuu akasema: “Je, mambo hayo ni ya kweli?” **2** Stefano akajibu: “Wanaume, akina ndugu na akina baba, sikilizeni. Mungu wa utukufu alimtokea babu yetu Abrahamu alipokuwa Mesopotamia, kabla hajaanza kuishi Harani,^b **3** naye akamwambia: ‘Ondoka katika nchi yako na kutoka kwa watu wako wa ukoo uje katika nchi nitakayoonyesha.’^c **4** Ndipo akaondoka katika nchi ya Wakaldayo, akaanza kuishi Harani. Na kutoka hapo, baada ya baba yake kufa,^d Mungu akamwagiza ahmie nchi hii ambayo mnaishi sasa.^e **5** Lakini hakumpa urithi wowote ndani

yake, hapana, hata sehemu ya kutosha kukanyaga kwa mguu; bali aliahidi atampa ai-miliki yeye na baada yake uzao wake,*^a ingawa bado ha-kuwa na mtoto. **6** Isitoshe, Mungu alimwambia kwamba wazao* wake wangukuwa wa-gezi katika nchi ambayo si yao na kwamba watu wa nchi hiyo wangewafanya kuwa wa-tumwa na kuwatesa* kwa mia-ka 400.^b **7** 'Nami nitalihuku-mu taifa hilo ambalo watali-tumikia,'^c Mungu akasema, 'na baada ya mambo hayo wata-toka na kunitolea utumishi mtakatifu mahali hapa.'^d

8 "Pia, alimpa agano la to-hara,^e naye Abrahamu akawa baba ya Isaka^f na kumtahiri siku ya nane,^g na Isaka akawa baba ya* Yakobo, naye Yako-bo akawa baba ya wale vichwa 12 vya familia.*^h **9** Na wale vi-chwa vya familia wakamwo-neo wivu Yosefu^h na kumu-za Misri.ⁱ Lakini Mungu ali-kuwa pamoja naye,^j **10** aka-mkomboa kutoka katika dhiki zake zote, akampa kibali na hekima mbele ya Farao mfal-me wa Misri. Naye Farao akamteua aongoze Misri na nyumba yake yote.^k **11** Laki-ni kukawa na njaa kali kati-ka nchi yote ya Misri na Kanaani, ndiyo, dhiki kuu, na mababu zetu hawakuwe-za kupata chakula chochote.^l **12** Lakini Yakobo akasikia kwamba kulikuwa na chaku-la* huko Misri, naye akawatu-ma mababu zetu mara ya kwa-nza.^m **13** Walipoenda mara

7:5 *Tnn., "mbegu yake." 7:6 *Tnn., "mbegu." #Au "kuwatendea vibaya." 7:8 *Au labda, "akafanya vivyo hivyo na." #Au "wazee wetu wa ukoo." 7:12 *Au "nafaka."

SURA YA 7

a Mwa 12:7
Mwa 13:14, 15
Mwa 17:1, 8

b Mwa 15:13
Kut 12:40

c Mwa 15:14

d Kut 3:12

e Mwa 17:9, 10

f Mwa 21:1-3

g Mwa 21:4

h Mwa 37:9-11

i Mwa 37:28
Mwa 45:4

j Mwa 39:2, 3

k Mwa 41:40-46

l Mwa 41:54
Mwa 42:5

m Mwa 42:2, 6

Safu ya 2

a Mwa 45:1, 16

b Mwa 45:9-11

c Mwa 46:27
Kum 10:22

d Mwa 46:29
Kum 26:5

e Mwa 49:33

f Kut 1:6

g Mwa 23:16
Kut 13:19
Yos 24:32

h Kut 1:7, 8

i Kut 1:10, 22

j Kut 2:2
Ebr 11:23

k Kut 2:3

l Kut 2:5, 10

m Kut 11:3

ya pili, Yosefu akajitambuli-sha kwa ndugu zake, naye Fa-rao akaifahamu familia ya Yo-sefu.^a **14** Basi Yosefu aka-watuma watu wamlete Yakobo baba yake na watu wake wote wa ukoo kutoka huko,^b jum-la ya watu* 75.^c **15** Ndipo Ya-kobo akashuka kwenda Mis-ri,^d naye akafa akiwa huko,^e na pia mababu zetu.^f **16** Wa-kabebwa mpaka Shekemu na kulazwa katika kaburi ambalo Abrahamu alikuwa amenu-nua kwa kiasi fulani cha fedha kutoka kwa wana wa Hamori huko Shekemu.^g

17 "Wakati ulipokuwa uki-karibia wa kutimizwa kwa ahadi ambayo Mungu alikuwa amempa Abrahamu, watu wa-kazidi kuongezeka huko Misri, **18** mpaka alipotokea mfalme mwingine huko Misri ambaye hakumjua Yosefu.^h **19** Mfal-me huyo akaitendea jamii yetu kwa hila na kuwalazimisha ki-makosa akina baba wawaa-che watoto wao wachanga ili wafe.ⁱ **20** Wakati huo Musa akazaliwa, naye alikuwa mwe-nye sura nzuri machoni pa Mungu. Akanyonyeshwa* kwa miezi mitatu nyumbani mwa baba yake.^j **21** Lakini ali-poachwa,*^k binti ya Farao akamchukua na kumlea kama mwana wake mwenyewe.^l **22** Basi Musa akafundishwa hekima yote ya Wamisri. Kwa kweli, alikuwa mwenye ngu-vu katika maneno na matendo yake.^m

23 "Sasa alipokuwa na umri wa miaka 40, wazo likai-ngia moyoni mwake* awate-

7:14 *Au "nafsi." 7:20 *Au "Akalele-wa." 7:21 *Au "alipotupwa." 7:23 *Au "akaamua."

mbelee* ndugu zake, wana wa Israeli.^a **24** Alipoona mmoja wao akitendewa isivyo haki, akamtetea na kulipiza kisasi kwa kumuua Mmisri. **25** Ali-dhani ndugu zake wangeelewa kwamba Mungu alikuwa aki-waokoa kupitia mkono wake, lakini hawakuelewa. **26** Siku iliyofuata aliwakuta wakipi-gana, akajaribu kuwapatani-sha kwa amani, akisema: 'Wanaume, ninyi ni ndugu. Kwa nini mnatendeanza vibaya?' **27** Lakini yule aliyekuwa akimtendea jirani yake viba-ya akamsukuma Musa na ku-mwambia: 'Ni nani aliyekuwe-ka uwe mtawala na mwamuzi wetu?' **28** Je, unataka kunuia kama ulivyomuua yule Mmisri jana?' **29** Aliposikia maneno hayo, Musa akakimbia na kwe-nda kuishi akiwa mgeni katika nchi ya Midiani, na huko aka-wa baba ya wana wawili.^b

30 "Baada ya miaka 40, malaika akamtokea kwenye nyi-ka ya Mlima Sinai katika mwali wa moto wa kichaka cha miiba kilichokuwa kikiwaka.^c **31** Musa alipoona jambo hilo, akashangaa sana. Laki-ni alipokaribia ili kuchungu-za, akasikia sauti ya Yehova* ikisema: **32** 'Mimi ni Mungu wa Mababu zako, Mungu wa Abrahamu na wa Isaka na wa Yakobo.'^d Musa akaanza kute-temeka na hakuthubutu ku-chunguza zaidi. **33** Yehova* akamwambia, 'Vua viatu vya-ko, kwa maana mahali una-posimama ni ardhi takatifu. **34** Hakika nimeona jinsi watu wangu walio Misri wanavyo-kandamizwa, nimesikia kilio

7:23 *Au "awakague." 7:31, 33 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 7

a Kut 2:11-15

b Kut 2:21, 22
Kut 18:2-4

c Kut 3:12-10

d Kut 3:6
Mk 12:26
Lu 20:37

Safu ya 2

a Kut 2:23, 24

b Kut 2:14
Mdo 7:27

c Kut 4:19

d Kut 12:41

e Kut 7:3

f Kut 14:21, 22
Kut 15:4, 5g Kut 16:35
Hes 14:33, 34h Kum 18:15
Mdo 3:22i Mdo 7:53
Gal 3:19j Kut 19:3
Kum 5:27k Kut 21:1
Kum 9:10

l Hes 14:3, 4

m Kut 16:3

n Kut 32:1, 23

o Kut 32:4, 6

p 2Fa 17:16

chao cha huzuni,^a nami ni-meshuka ili kuwaokoa. Basi njoo, nitakutuma huko Misri.'

35 Huyu Musa ambaye wali-mkana wakisema: 'Ni nani aliyekuweka uwe mtawala na mwamuzi?'^b ndiye ambaye Mungu alimtuma^c akiwa mta-wala na mkombozi kupitia malaika aliyemtokea katika kichaka cha miiba. **36** Yeye ndiye aliyewaongoza wato-ke huko,^d akifanya mambo ya ajabu* na ishara huko Misri^e na kwenye Bahari Nyekundu^f na nyikani kwa miaka 40.^g

37 "Huyu ndiye Musa aliye-waambia hivi wana wa Israe-li: 'Mungu atawainulia na-bii kama mimi kutoka kati ya ndugu zenu.'^h **38** Huyu ndi-ye aliyekuwa kati ya kutani-ko huko nyikani pamoja na malaikaⁱ aliyezungumza naye/^j kwenye Mlima Sinai na ma-babu zetu, naye akapokea ma-neno matakatifu yaliyo hai ili atupatie.^k **39** Mababu zetu walikataa kumtii, badala yake wakampuuza^l na katika moyo yao wakarudi Misri,^m **40** wa-kimwambia Haruni: 'Tutenge-neeze miungu itakayotuongo-za. Kwa sababu hatujui lili-lompata huyu Musa aliye-tuongoza kutoka nchi ya Misri.'ⁿ **41** Ndipo wakatenge-geza ndama siku hizo na kui-letea sanamu hiyo dhabihu nao wakaanza kufurahia kazi za mikono yao.^o **42** Basi Mu-ngu akageuka na kuwaacha, akawakabidhi watoe utumishi mtakatifu kwa jeshi la mbi-nguni,^p kama vile ilivyoandi-kwa katika kitabu cha Mana-bii: 'Enyi nyumba ya Israe-li, je, mimi ndiye mliyetolea

7:36 *Au "miujiza."

matoleo na dhahibu nyikani kwa miaka 40? **43** Bali mlichukua hema la Moloki^a na nyota ya mungu Refani, sanamu mlizotengeneza ili kuziambudu. Kwa hiyo nitawahamishia ng'ambo ya Babiloni.^b

44 "Mababu zetu walikuwa na hema la ushahidi nyikani, lililotengenezwa kwa kufuata maagizo ambayo Mungu alimpa Musa kulingana na mfano alikuwa amemwonesha.^c **45** Nao mababu zetu wakalimiliki na kulileta pamoja na Yoshua kwenye nchi iliyomilikiwa na mataifa,^d ambayo Mungu aliyafukuza kutoka mbele ya mababu zetu.^e Nalo likakaa huko mpaka siku za Daudi. **46** Alipata kibali machoni pa Mungu naye akaomba pendeleo la kujenga makao kwa ajili ya Mungu wa Yakobo.^f **47** Lakini Sulemani ndiye aliyemjengea nyumba.^g **48** Hata hivyo, Aliye Juu Zaidi haishi katika nyumba zilizojengwa kwa mikono,^h kama vile nabii anavyosema: **49** 'Mbingu ni kiti changu cha ufalme,ⁱ nayo dunia ni kiti cha miguu yangu.^j Mtanijengea nyumba ya aina gani? Asema Yehova.* Au pako wapi mahali pangu pa kupumzikia? **50** Mkono wangu uliumba vitu hivi vyote, sivyo?"^k

51 "Ninyi watu wagumu na wasiotahiriwa katika mioyo na masikio, sikuzote mnaipinga roho takatifu; kama mababu zenu walivyofanya, ndivyo mnavyofanya pia.^l **52** Ni yupi kati ya manabii ambaye mababu zenu hawakumtesa?^m Ndiyo, waliwaua wale waliota-

SURA YA 7

a 1Fa 11:7

b Yer 25:11
Amo 5:25-27

c Kut 25:40

d Kum 3:28
Kum 31:3
Yos 3:14e Mwa 17:1, 8
Yos 23:9
Yos 24:18f 2Sa 7:2
1Nya 22:7
Zb 132:1-5

g 1Fa 6:1

h Mdo 17:24

i Zb 11:4

j Mt 5:34, 35

k Isa 66:1, 2
Ebr 3:4

l Isa 63:10

m 2Nya 36:16

Safu ya 2

a Mt 23:31

b Isa 53:8
Mdo 3:13, 14c Mdo 7:38
Gal 3:19d Zb 110:1
Mt 26:64

e Da 7:13

f Ro 8:34

g Law 24:14, 16
Mt 23:37
Yoh 16:2

h Kum 17:7

i Mdo 8:1
Mdo 22:20

j Mt 5:44

SURA YA 8

k Mdo 7:58

l Mt 10:23
Mdo 11:19

ngaza mapema kuhusu kuja kwa yule mwadilifu,^a ambaye ninyi mmemsaliti na kumuua,^b **53** ninyi mliopokea Sheria kupitia malaika^c lakini hamkuishika."

54 Basi, waliposikia mambo hayo wakawaka hasira* moyoni na kuanza kumsagia meno yao. **55** Lakini Stefano akiwa amejaa roho takatifu, akatazama mbinguni, akao na utukufu wa Mungu na wa Yesu akiwa amesimama kwenye mkono wa kuume wa Mungu,^d **56** naye akasema: "Tazama! Ninazona mbingu zimefunguka na Mwana wa binadamu^e akiwa amesimama kwenye mkono wa kuume wa Mungu."^f

57 Ndipo wakapaza sauti ya juu na kuziba masikio kwa mikono yao, wote wakamrukia kwa pamoja. **58** Baada ya kumtupa nje ya jiji, wakaanza kumpiga mawe.^g Wale mashahidi^h wakaweka mavazi yao ya nje miguuni pa kijana aliyeitwa Sauli.ⁱ **59** Walipokuwa wakimpiga mawe Stefano, akaomba hivi: "Bwana Yesu, pokea roho yangu." **60** Kisha akapiga magoti, akasema kwa sauti kubwa: "Yehova,* usiwahe sabie dhambi hii."^j Na baada ya kusema hayo, akalala usingizi katika kifo.

8 Naye Sauli aliunga mkono kuuawa kwa Stefano.^k

Kuanzia siku hiyo kutaniko lililokuwa Yerusalemu likaaanza kuteswa sana; wanafunzi wote isipokuwa mitume wakatawanyika kotekote katika maeneo ya Yudea na Samaria.^l **2** Lakini wanaume waliomwogopa Mungu waka-

mbeba Stefano ili wakamzike, nao wakamwombolezea sana. **3** Ndipo Sauli akaanza kuli-shambulia kutaniko. Alikuwa akivamia nyumba moja baada ya nyingine, akiwakokota nje wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani.^a

4 Hata hivyo, wale waliotawanyika wakapita katika nchi wakitangaza habari njema ya lile neno.^b **5** Sasa Filipo akashuka kwenda jiji la Samaria*^c akaanza kuwahubiria kumhusu Kristo. **6** Umati wote kwa pamoja ulikazia fikira mambo ambayo Filipo alikuwa akisema huku wakisikiliza na kutazama ishara alizokuwa akifanya. **7** Kwa maana wengi walikuwa na roho waovu, na roho hao walipaza sauti kubwa na kutoka.^d Isitoshe, wengi waliokuwa wamepooza na vilema waliponywa. **8** Basi kukawa na shangwe kubwa sana katika jiji hilo.

9 Katika jiji hilo kulikuwa na mwanamume aliyelitwa Simoni, ambaye kabla ya hapo alikuwa akifanya uchawi na kulishangaza taifa la Samaria, akidai kwamba alikuwa mtu mkuu. **10** Watu wote, kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi walimkazia fikira na kusema: "Mtu huyu ndiye Nguvu za Mungu, zinazoitwa Kuu." **11** Basi walikuwa wakimsikiliza kwa sababu alikuwa amewashangaza kwa muda fulani kwa uchawi wake. **12** Lakini walipomwamini Filipo, aliyekuwa akitangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu^e na kuhusu jina la Yesu Kristo, wanaume na pia wana-

8:5 *Au labda, "mojawapo ya majiji ya Samaria."

SURA YA 8

a Mdo 9:1, 2
Mdo 22:4
Mdo 26:10
Gal 1:13
Flp 3:5, 6

b Mdo 11:19

c Yoh 4:39-42
Mdo 1:8

d Mt 10:1
Mk 6:7

e Lu 8:1

Safu ya 2

a Mt 28:19
Mdo 18:8

b Mdo 6:5

c Mdo 11:1

d Mt 16:19

e Mdo 10:47, 48
Mdo 19:2, 3

f Mdo 6:5, 6
Mdo 19:6
ZTi 1:6

g Mt 10:8
Mdo 10:45

wake wakabatizwa.^a **13** Simoni pia akawa mwamini na baada ya kubatizwa, akaandamana na Filipo;^b naye alishangaa kuona ishara na matendo yenye nguvu yaliyokuwa yakifanywa.

14 Mitume huko Yerusalemu waliposikia kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu,^c wakawatuma Petro na Yohana kwao; **15** nao wakashuka kwenda huko, wakasali kwa ajili yao ili wapate roho takatifu.^d **16** Kwa maana bado haikuwa imekuja juu ya yeyote kati yao, bali walikuwa wamebatizwa tu katika jina la Bwana Yesu.^e **17** Ndipo wakaweka mikono juu yao,^f nao wakaanza kupokea roho takatifu.

18 Simoni alipoona kwamba watu walipokea roho takatifu mitume walipoweka mikono juu yao, akawatolea pesa, **19** akawaambia: "Nipeni mimi pia mamlaka hii, ili yeyote nitakayeweka mikono juu yake apokee roho takatifu." **20** Lakini Petro akamwambia: "Fedha yako na iangamie pamoja nawe, kwa sababu ulidhani utanunua zawadi ya bure ya Mungu kwa kutumia pesa.^g **21** Wewe huna sehemu wala fungu katika jambo hili, kwa maana moyo wako si mnyoofu machoni pa Mungu. **22** Basi tubu huu ubaya wako, na umwombe Yehova* dua, ili ikiwezekana, usamehewe nia mbaya ya moyo wako; **23** kwa maana ninao-na wewe ni sumu chungu* na mtumwa wa ukosefu wa

8:22 *Angalia Nyongeza A5. 8:23 *Tnn., "nyongo ya uchungu."

uadilifu.” **24** Simoni aka-waambia: “Mwombeni Yehova* dua kwa ajili yangu ili nisi-patwe na lolote kati ya mambo mliyosema.”

25 Kwa hiyo, baada ya kutoa ushahidi kamili na kulisema neno la Yehova,* wakaanza kurudi Yerusalemu, nao wakaenda wakitangaza habari njema katika vijiji vingi vya Wasamaria.^a

26 Hata hivyo, malaika^b wa Yehova* akamwambia Filipo: “Ondoka uende kusini kwenye barabara inayoshuka kutoka Yerusalemu kwenenda Gaza.” (Hii ni barabara ya jangwani.) **27** Ndipo akaondoka na kwenda, na tazama! akamwona towashi* Mwe-thiopia, mwanamume aliyekuwana na mamlaka chini ya Kandake, malkia wa Waethiopia, na ambaye alisimamia hazina yote ya malkia. Alikuwa ameenda Yerusalemu kuabudu,^c **28** naye alikuwa akirudi akiwa ameketi kwenye gari lake, akisoma kwa sauti kubwa maandishi ya nabii Isaya. **29** Basi roho ikamwambia Filipo: “Nenda ukaribie gari hilo.” **30** Filipo akakimbia kandokando na kumsikia akisoma kwa sauti kubwa maandishi ya nabii Isaya, akamuuliza: “Je, kweli unajua* unayosoma?” **31** Akajibu: “Kwa kweli, ninawezaje kuyaelewa mtu fulani asiponiongoza?” Basi akamsihi Filipo apande aketi pamoja naye. **32** Alikuwa akisoma kifungu hiki cha Andiko: “Kama kondoo, alipelekwa machinjioni, na kama

8:24-26, 39 *Angalia Nyongeza A5.
8:27 *Au “ofisa wa makao ya mfalme.”
8:30 *Au “unaelewa.”

SURA YA 8

a Mt 9:35
Mdo 1:8

b Ebr 1:7, 14
Ufu 14:6

c 2Nya 6:32, 33

Safu ya 2

a 1Pe 2:23

b Mt 26:59

c Isa 53:7, 8
Da 9:26
Flp 2:8

d Mdo 21:8

SURA YA 9

e Mdo 8:3
Mdo 22:4
Mdo 26:10, 11
Gal 1:13
1Ti 1:12, 13

f Mdo 11:26
Mdo 22:4

mwanakondoo aliye kimya mbele ya mtu anayemnyoa, vivyo hivyo yeye hafungui kinywa chake.^a **33** Alipokuwa akiabishwa, hakutendewa kwa haki.^b Ni nani atakayeeleza habari za kizazi chake? Kwa sababu uhai wake unao-ndolewa duniani.”^c

34 Ndipo yule towashi akamwambia Filipo: “Tafadhali niambie, nabii anasema hivyo kumhusu nani? Kuhusu yeye mwenyewe au mtu mwingine?” **35** Filipo akaanza kuzungumza, akianza na andiko hilo akamtangazia habari njema kumhusu Yesu. **36** Wakiwa kwenye ile barabara, wakafika mahali penye maji, na towashi akasema: “Tazama! Hapa kuna maji; ni nini kinachonizuia kubatizwa?” **37** * — **38** Ndipo akaamuru gari lisimame, na wote wawili Filipo na towashi wakaingia ndani ya maji, naye akambatiza. **39** Walipopanda kutoka ndani ya maji, roho ya Yehova* ikamwongoza Filipo upesi aondoke, na towashi hakumwona tena, bali aliendelea na safari yake aki-shangilia. **40** Hata hivyo, Filipo akajikuta huko Ashdodi, naye akapita katika eneo hilo, akaendelea kuyatangazia habari njema majiji yote mpaka alipofika Kaisaria.^d

9 Lakini Sauli aliendelea kuwatisha wanafunzi wa Bwana akitaka kuwaua,^e basi akamwendea kuhani mkuu **2** na kumwomba barua za kwenda kwenye masinagogi huko Damasko, ili awakamate wanaume na wanawake walioifuata Ilea Njia,^f na kuwale-

8:37 *Angalia Nyongeza A3.

ta Yerusalemu wakiwa wamefungwa.

3 Akiwa safarini karibu ku-fika Damasko, ghafla nuru kutoka mbinguni ikamulika kumzunguka.^a **4** naye akaanguka chini na kusikia sauti ikimwambia: "Sauli, Sauli, kwa nini unanitesa?" **5** Akauliza: "Wewe ni nani Bwana?" Akajibu: "Mimi ni Yesu,^b ambaye unamtesa.^c **6** Hata hivyo, inuka uende jijini, nawe utamibiwa unachopaswa kufanya."

7 Wanaume waliokuwa wakisafiri pamoja naye walisimama wakiwa hawana la kusema, kwa kweli waliisikia sauti, lakini hawakumwona mtu yeyote.^d **8** Kisha Sauli akainuka, na ingawa macho yake yalikuwa yamefunguka, hangeweza kuona chochote. Basi wakamshika mkono na kumwongoza mpaka Damasko. **9** Na kwa siku tatu hakuona chochote,^e na hakula wala kunywa.

10 Huko Damasko kulikuwa na mwanafunzi aliyelitwa Anania,^f naye Bwana akamwambia katika maono: "Anania! Akajibu: "Mimi hapa, Bwana." **11** Bwana akamwambia: "Ondoka, uende kwenye barabara inayoitwa Nyoofo, umtafute mwanamume anayelitwa Sauli, kutoka Tarso,^g kwenye nyumba ya Yuda. Kwa maana tazama! anasali, **12** na katika maono amemwona mwanamume anayelitwa Anania akiingia na kuweka mikono juu yake ili aweze kuona tena."^h

13 Lakini Anania akajibu: "Bwana, nimesikia kutoka kwa watu wengi kuhusu mtu huyu, jinsi alivyowatesa watakatifu wako huko Yerusalemu.

SURA YA 9

a Mdo 22:6-11
Mdo 26:13-18

b 1Ko 15:8

c Mt 25:45

d Mdo 22:9

e Mdo 13:11

f Mdo 22:12

g Mdo 21:39
Mdo 22:3

h Mdo 9:17

Safu ya 2

a Mdo 9:1, 2

b Mdo 13:2
Ro 1:1
1Ti 1:12

c Ro 1:5
Gal 2:7
1Ti 2:7

d Mdo 26:1
Mdo 27:24

e Mdo 20:22, 23
Mdo 21:11
2Ko 11:23-28
Kol 1:24
2Ti 1:12

f Mdo 22:12, 13

g Mdo 26:19, 20

h Mdo 8:3
Gal 1:13, 23

i Mdo 9:1, 2

j Mdo 17:2, 3

14 Na sasa amepewa mamla-ka na wakuu wa makuhani ili awakamate* wote wanaoliitia jina lako."^a **15** Lakini Bwana akamwambia: "Nenda! kwa sababu mtu huyu ni chombo nilichokichagua^b ili kupeleka jina langu kwa mataifa^c na pia kwa wafalme^d na wana wa Israeli. **16** Kwa maana nitamwonyesha waziwazi mateso mengi yatakayompata kwa sababu ya jina langu."^e

17 Basi Anania akaenda na kuingia katika ile nyumba, naye akaweka mikono yake juu ya Sauli na kusema: "Sauli, ndugu, Bwana Yesu aliyekutokea barabarani ulipokuwa ukija, amenituma ili uweze kuona tena na ujazwe roho takatifu."^f **18** Papo hapo, vitu kama magamba vikaanguka kutoka katika macho yake, naye akaanza kuona tena. Kisha akasimama na kubatizwa, **19** naye akala chakula na kupata nguvu.

Akakaa kwa siku kadhaa pamoja na wanafunzi huko Damasko,^g **20** na mara moja akaanza kuhubiri katika masinagogi kuhusu Yesu, kwamba huyo ndiye Mwana wa Mungu. **21** Wote waliomsikia wakashangaa na kusema: "Je, huyu si yule mtu aliyewashambulia wale wanaoliitia jina hilo huko Yerusalemu?"^h Je, hakuja huku ili awakamate na kuwapeleka* kwa wakuu wa makuhani?"ⁱ **22** Lakini Sauli akazidi kupata nguvu na kuwashangaza Wayahudi walioishi Damasko, akithibitisha kupatana na akili kwamba huyu ndiye Kristo.^j

9:14 *Tnn., "awafunge; awatie vifungoni." **9:21** *Tnn., "kuwangoza wakiwa wamefungwa."

23 Baada ya siku nyingi kupita, Wayahudi wakapanga njama pamoja ili kumuua.^a

24 Hata hivyo, Sauli akagundua njama yao. Pia walikuwa wakilinda malango usiku na mchana ili wamuue. **25** Basi wanafunzi wake wakamchukua na kumshusha usiku kupitia shimo ukutani, akiwa ndani ya kapu.^b

26 Alipofika Yerusalemu,^c akajaribu kujiunga na wanafunzi, lakini wote walimwogopa kwa sababu hawakumini kwamba amekuwa mwanafunzi. **27** Ndipo Barnaba^d akamsaidia na kumpeleka kwa mitume, naye akawasimulia kirefu jinsi alivyokuwa amemwona Bwana^e barabarani, na kwamba alikuwa amezungumza naye, na jinsi alivyozungumza kwa ujasiri katika jina la Yesu^f huko Damasko. **28** Basi akakaa pamoja nao, akitembea kwa uhuru* huko Yerusalemu, akizungumza kwa ujasiri katika jina la Bwana. **29** Alikuwa akiongea na kubishana na Wayahudi waliozungumza Kigiriki, lakini hao walikuwa wakijaribu kumuua.^g **30** Akina ndugu walipogundua hilo, wakampeleka Kaisaria na kumtuma aende Tarso.^h

31 Ndipo kutaniko katika eneo lote la Yudea, Galilaya, na Samariaⁱ likaingia katika kipindi cha amani, huku likijengwa; nalo lilipokuwa likitembea katika kumwogopa Yehova* na katika faraja ya roho takatifu,^j likaendelea kuingezeka.

9:28 *Tnn., "akiingia na kutoka." 9:31 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 9

a Mdo 20:2, 3
Mdo 23:12
2Ko 11:23

b 2Ko 11:32, 33

c Gal 1:18

d Mdo 4:36, 37

e Mdo 9:3, 4
1Ko 9:1

f Mdo 9:19, 20

g 2Ko 11:23, 26

h Mdo 11:25
Gal 1:21

i Mdo 8:1

j Yoh 14:16

Safu ya 2

a Mdo 9:38

b Mt 10:8
Mdo 4:9, 10

c Mdo 3:6

d Lu 8:51

32 Petro alipokuwa akisafiri katika eneo hilo lote, akashuka pia kwa watakatifu walioishi Lida.^a **33** Huko akampata mwanamume aliyetwa Ainea, ambaye alikuwa amelala kwenye kitanda chake kwa miaka minane, kwa maana alikuwa amepooza. **34** Petro akamwambia: "Ainea, Yesu Kristo anakuponya.^b Simama, utandike kitanda chako."^c Naye akasimama mara moja. **35** Wote walioishi huko Lida na katika Nchi Tambarare ya Sharoni walipomwona, wakamgeukia Bwana.

36 Huko Yopa kulikuwa na mwanafunzi aliyetwa Tabitha, jina ambalo linapotafsiriwa linamaanisha "Dorkasi."^{*} Alikuwa akitenda mateendo mema na kutoa zawadi za rehema. **37** Lakini siku hizo akawa mgonjwa, akafa. Basi wakamwsha na kumlaza katika chumba cha juu. **38** Kwa kuwa Lida ilikuwa karibu na Yopa, wanafunzi waliposikia kwamba Petro alikuwa katika jiji hilo wakatuma wanaume wawili wakamsihi: "Tafadhali njoo kwetu haraka iwezekanavyo." **39** Ndipo Petro akainuka na kwenda pamoja nao. Alipofika, wakampeleka kwenye kile chumba cha juu; nao wajane wote wakaja kwake wakilia na kuonyesha mavazi mengi na majoho* ambayo Dorkasi alikuwa ametengeneza alipokuwa pamoja nao. **40** Petro akaagiza kila mtu aende nje,^d akapiga magoti na kusali. Kisha akaageukia ule mwili, akasema: "Tabi-

9:36 *Jina la Kigiriki Dorkasi na jina la Kiaramu Tabitha, yote yanamaanisha "Swala." 9:39 *Au "mavazi ya nje."

tha, inuka!" Akafungua macho yake, na alipomwona Petro, akaketi.^a **41** Petro akamshika mkono na kumwinua, akawaita watakatifu na wajane, akamkabidhi kwao akiwa hai.^b **42** Jambo hilo likajulikana kotekote huko Yopa, na wengi wakamwamini Bwana.^c **43** Petro akakaa Yopa siku kadhaa pamoja na mtengenezaji wa ngozi aliyelitwa Simoni.^d

10 Sasa huko Kaisaria kulikuwa na mwanamume aliyelitwa Kornelio, ofisa wa jeshi* wa kikosi# cha Italia. **2** Alikuwa mtu aliyemheshimu na kumwogopa Mungu, yeye pamoja na watu wote wa nyumba yake, naye aliwapa watu zawadi nyingi za rehema na aliomba dua siku zote kwa Mungu. **3** Karibu saa tisa^e mchana* aliona waziwazi katika maono malaika wa Mungu akija na kumwita: "Kornelio!" **4** Kornelio akamkazia macho, akiwa na hofu, na kumuuliza: "Kuna nini, Bwana?" Akamwambia: "Mungu amesikia sala zako na kuona zawadi zako za rehema, naye anazikumbuka.^f **5** Basi sasa tuma watu huko Yopa wakamwite Simoni anayelitwa Petro. **6** Mtu huyo ni mgeni wa Simoni, mtengenezaji wa ngozi, aliye na nyumba kando ya bahari." **7** Mara tu yule malaika aliyezungumza naye alipoondoka, akawaita wawili kati ya watumishi wake na mmoja wa wanajeshi wake aliyemwogopa Mungu,

10:1 *Ofisa aliyesimamia wanajeshi 100. #Kikosi cha jeshi la Roma chenye wanajeshi 600. **10:3** *Yaani, karibu saa 9 alasiri.

SURA YA 9

a Mt 9:24, 25
Lu 7:14, 15
Yoh 11:43, 44

b 1Fa 17:23

c Yoh 11:44, 45

d Mdo 10:6, 32

SURA YA 10

e Mdo 3:1

f Zb 65:2

Safu ya 2

a Mdo 11:5-10

b Law 11:4
Law 11:13-20
Law 20:25
Kum 14:3, 19
Eze 4:14

c Mdo 11:11

d Mdo 13:2
Mdo 15:28
Mdo 16:6
Mdo 20:23

8 naye akawasimulia mambo yote, kisha akawatuma wae-nde Yopa.

9 Siku iliyofuata, wakiwa safarini karibu kufika kwenye jiji hilo, Petro alipanda kwenye paa la nyumba karibu saa sita* ili kusali. **10** Lakini akahisi njaa sana na akatamani kula. Walipokuwa wakitayarisha mlo, akapata njozi^a **11** naye akaona mbingu imefunguliwa na kitu fulani* kikishuka kama shuka kubwa la kitani, kikiteremshwa dunia ni kwa ncha zake nne; **12** na ndani yake mlikuwa na kila aina ya wanyama wenyewe miguu minne, viumbe wanaotambaa wa dunia, na ndege wa angani. **13** Kisha sauti ikamwambia: "Petro, simama, chinja ule!" **14** Lakini Petro akajibu: "Hapana Bwana, kwa maana sijawahi kula kitu chochote kilicho najisi na kisicho safi."^b **15** Ile sauti ikamwambia mara ya pili: "Acha kuvitita najisi vitu ambavyo Mungu amevitakasa." **16** Jambo hilo likatokea mara ya tatu, na papo hapo kile chombo kika-rudishwa mbinguni.

17 Petro akiwa bado anashangaa kuhusu maana ya maono hayo, wakati huohuo wale watu waliotumwa na Kornelio waliulizia nyumba ya Simoni nao walikuwa wamesimama langoni.^c **18** Nao wakaita kwa sauti na kuuliza ikiwa Simoni anayelitwa Petro alikuwa mgeni humo. **19** Petro alipokuwa akiwaza kuhusu yale maono, roho^d ikasema: "Tazama!

10:9 *Yaani, karibu saa 6 mchana. **10:11** *Tnn., "chombo cha aina fulani."

Wanaume watatu wanakuta-futa. **20** Basi simama, ushuke na kwenda pamoja nao, usiwe na shaka kamwe, kwa sababu nimewatuma.” **21** Kisha Petro akashuka kutoka ghorofani akawaambia wale wanaume: “Mimi ndiye mna-yenitafuta. Kwa nini mmekuja hapa?” **22** Wakajibu: “Kornelio,^a ofisa wa jeshi, mwana-mume mwadilifu anayemwo-gopa Mungu na mwenye sifa njema katika taifa lote la Wayahudi, alipewa maagizo na Mungu kupitia malaika mtakatifu kwamba awatume watu wakuite uje nyumbani kwa-ke ili wasikie mambo utakayo-sema.” **23** Basi akawakaribi-sha na kukaa nao.

Siku iliyofuata Petro akaon-doka pamoja nao, na baa-dhi ya akina ndugu wa huko Yopa wakaenda pamoja naye. **24** Kesho yake akafika Kaisa-ria. Bila shaka, Kornelio alikuwa akiwatarajia naye alikuwa amekusanya watu wake wa ukoo na rafiki zake wa kari-bu. **25** Petro alipokuwa akiingia, Kornelio akamlaki, akapiga magoti miguuni pake, na kumsujudia.* **26** Lakini Petro akamwinua, akisema: “Si-mama; mimi pia ni mwanadamu tu.”^b **27** Alipokuwa aki-zungumza naye akaingia na kuwakuta watu wengi wamekusanyika. **28** Akawaambia: “Mnajua jinsi ilivyo kinyume cha sheria kwa Myahudi ku-shirikiana au kumkaribia mtu wa jamii nyingine,^c lakini Mungu amenionyesha kwamba si-paswi kumwita mtu yeyote na-jisi au asiye safi.^d **29** Basi ni-lipoitwa nilikuja bila kupinga.

10:25 *Au “kumwinamia.”

SURA YA 10

a Mdo 10:1

b Lu 4:8
Mdo 14:12-15
Ufu 19:10
Ufu 22:8, 9

c Yoh 18:28

d Mdo 10:45
Efe 3:5, 6

Safu ya 2

a Mdo 9:43

b Kum 10:17
2Nya 19:7
Ro 2:11

c Ro 2:13
1Ko 12:13
Gal 3:28

d Isa 52:7
Nah 1:15

e Mt 28:18
Ro 14:9
Ufu 19:11, 16

f Lu 4:14

g Isa 11:2
Isa 42:1
Isa 61:1
Mt 3:16

Kwa hiyo ninawauliza: ‘Kwa nini mmeniita?’”

30 Ndipo Kornelio akase-ma: “Siku nne zilizopita wa-kati kama huu, nilikuwa niki-sali katika nyumba yangu saa tisa;* wakati huohuo mwana-mume aliyevaa mavazi yana-yong’aa akasimama mbele ya-angu **31** na kusema: ‘Korne-lio, sala yako imesikiwa na kukubaliwa, naye Mungu ame-zikumbuka zawadi zako za re-hema. **32** Kwa hiyo, tuma watu waende Yopa waka-mwite Simoni anayeitwa Pe-tro. Mtu huyu ni mgeni katika nyumba ya Simoni, mtengenezaji wa ngozi, kando ya bahari.’^a **33** Mara moja ni-kawatuma watu kwako, nawe umefanya vizuri kuja hapa. Basi sote tupo mbele za Mu-ngu ili kuyasikia mambo yote ambayo Yehova* amekuamuru useme.”

34 Ndipo Petro akaanza ku-zungumza, akasema: “Kwa ha-kika ninaona kwamba Mungu hana ubaguzi,^b **35** lakini ka-tika kila taifa mtu anayemwo-gopa na kutenda uadilifu ana-kubaliwa naye.^c **36** Alituma ujumbe kwa wana wa Israe-li akiwatangazia habari njema ya amani^d kupitia Yesu Kristo —huyu ndiye Bwana wa wote.^e **37** Mnajua habari iliyozungu-mzwa kotekote huko Yu-dea, kuanzia Galilaya^f baada ya ubatizo aliohubiri Yohana: **38** kumhusu Yesu aliyetoka Nazareti, jinsi Mungu alivyo-mtia mafuta kwa roho taka-tifu^g na nguvu, naye akapi-ta katika nchi akitenda mema na kuwaponya wote walioka-

10:30 *Yaani, karibu saa 9 alasiri.
10:33 *Angalia Nyongeza A5.

ndamizwa na Ibilisi,^a kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye.^b **39** Nasi ni mashahidi wa mambo yote aliyofanya katika nchi ya Wayahudi na huko Yerusalemu; lakini walimuua kwa kumtundika kwenye mti. **40** Mungu alimfufua siku ya tatu^c na kumfufua,* **41** si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliochaguliwa awali na Mungu, kwe-tu sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuliwa kutoka kwa wafu.^d **42** Pia, alituumuru tuwahubirie watu na kutoa ushahidi kamili^e kwamba yeye ndiye aliyeagizwa na Mungu kuwa mwamuzi wa walio hai na wafu.^f **43** Manabii wote wali-toa ushahidi^g kumhusu, kwamba kila mtu anayemwamini hupokea msamaha wa dhambi kupitia jina lake.^h

44 Petro alipokuwa akizungumza kuhusu mambo hayo, roho takatifu ikaja juu ya wote waliokuwa wakisikia lile neno.ⁱ **45** Nao waamini* waliotahiriwa ambao walikuwa wamekuja pamoja na Petro wakashangaa, kwa sababu zawadi ya bure ya roho takatifu ilikuwa ikimiminwa pia juu ya watu wa mataifa. **46** Kwa maana waliwasikia wakizungumza lugha* za wageni na kumtukua Mungu.^j Ndipo Petro akauliza: **47** “Je, kuna yeyote anayeweza kuwazuia hawa waliopokea roho takatifu kama tulivyoipokea wasibatizwe^k kwa maji?” **48** Ndipo akawaamuru wabatizwe katika jina la Yesu Kristo.^l Ki-

10:40 *Au “kumfanya aonekane.”
10:45 *Au “waaminifu.” **10:46** *Tnn., “ndimi.”

SURA YA 10

a Lu 13:16

b Yoh 3:1, 2

c Yon 1:17
Yon 2:10
Mdo 2:23, 24d Lu 24:30, 31
Yoh 21:13, 14e Mt 28:19, 20
Mdo 1:8f Mdo 17:31
Ro 14:9
2Ko 5:10
2Ti 4:1
1Pe 4:5g Lu 24:27
Ufu 19:10h Isa 53:11
Yer 31:34
Da 9:24i Mdo 4:31
Mdo 8:14, 15j Mdo 2:1, 4
Mdo 19:6k Mt 3:11
Mdo 8:36
Mdo 11:17l Mt 16:19
Mdo 2:38

Safu ya 2

SURA YA 11

a Mdo 10:45
Gal 2:12

b Mdo 10:10-16

sha wakamwomba akae pamoja nao siku kadhaa.

11 Sasa mitume na ndugu waliokuwa Yudea wakisikia kwamba watu wa mataifa pia walikuwa wamelikubali neno la Mungu. **2** Basi Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale waliounga mkono kutahiriwa^a wakaanza kumkosoa,* **3** wakisema: “Uliingia ndani ya nyumba ya watu ambao hawajatahiriwa nawe ukala pamoja nao.” **4** Ndipo Petro akawafafanulia jambo hilo kwa kina, akisema:

5 “Nilipokuwa nikisali katika jiji la Yopa, niliona maono katika njozi, kitu fulani* kiki-shuka kama shuka kubwa la kitani, kikiteremshwa kutoka mbinguni kwa ncha zake nne, nacho kikaja moja kwa moja mpaka mahali nilipokuwa.^b

6 Nilipotazama kwa makini ndani yake, nikaona wanyama wa dunia wenye miguu minne, wanyama wa mwituni, viumbe wanaotambaa, na ndege wa angani. **7** Pia nikasikia sauti ikiniambia: ‘Petro, simama, chinja ule!’ **8** Lakini nikasema, ‘Hapana Bwana, kwa sababu kitu chochote najisi au kisicho safi hakijawahi kamwe kuingia kinywani mwangu.’ **9** Mara ya pili, ile sauti kutoka mbinguni ikajibu: ‘Wewe acha kuvuita najisi vitu ambavyo Mungu amevitakasa.’ **10** Hilo likatokea mara ya tatu, na kila kitu kikavutwa juu kuru-di mbinguni. **11** Wakati huo-huo, wanaume watatu walio-tumwa kwangu kutoka Kaisaria walikuwa wamesimama

11:2 *Au “kushindana naye.” **11:5** *Tnn., “chombo cha aina fulani.”

karibu na nyumba tuliyokuwa tukikaa.^a **12** Ndipo roho ikaniambia niende pamoja nao, bila kuwa na shaka hata kidogo. Lakini hawa ndugu sita pia walienda pamoja nami, nasi tukiangia ndani ya nyumba ya mwanamume huyo.

13 "Alitueleza jinsi alivyomwona malaika akiwa amesimama katika nyumba yake na kumwambia, 'Watume watu waende Yopa wakamwite Simoni anayeitwa Petro,^b **14** naye atakuambia mambo yatayokusaidia wewe na watu wote wa nyumba yako mwokolewe.' **15** Lakini nilipoanza kuzungumza, roho takatifu ikaja juu yao kama ilivyokuja juu yetu mwanzoni.^c **16** Ndiipo nikakumbuka maneno aliyokuwa akisema Bwana: 'Yohana alibatiza kwa maji,^d lakini ninyi mtabatizwa kwa roho takatifu.'^e **17** Kwa hiyo, ikiwa Mungu aliwapa zawadi ileile ya bure kama alivyotupatia sisi ambao tumemwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani hata niweze kumzuia* Mungu?"^f

18 Waliposikia mambo hayo, wakaacha kupinga,* nao wakamtukuza Mungu wakisema: "Kwa hiyo basi, Mungu pia ameruhusu watu wa mataifa watubu ili wapate uzima."^g

19 Sasa wale waliokuwa wametawanyika^h kwa sababu ya dhiki iliyotokea kuhusiana na Stefano, wakaenda mpaka Foinike, Kipro, na Antiokia, lakini walitangaza lile neno kwa Wayahudi tu.ⁱ **20** Hata hivyo, wanaume fulani kati

11:17 *Au "kumpinga." 11:18 *Tnn., "wakanyamaza."

SURA YA 11

a Mdo 10:17-20

b Mdo 10:30-33

c Mdo 2:1, 4
Mdo 10:44, 45d Mt 3:11
Mk 1:8
Lu 3:16
Mdo 1:5e Yoe 2:28
Yoh 1:33
Mdo 2:17

f Mdo 10:47

g Isa 11:10
Mdo 17:30
Ro 10:12
Ro 15:8, 9

h Mdo 8:1

i Mt 10:5, 6

Safu ya 2

a Mdo 2:47
Mdo 9:35

b Mdo 4:36, 37

c Mdo 13:43
Mdo 14:21, 22d Mdo 2:47
Mdo 4:4
Mdo 5:14
Mdo 9:31

e Mdo 21:39

f Mdo 9:2

g Iko 12:28
Efe 4:11

h Mdo 21:10, 11

i Mt 24:7

j 2Ko 8:12

k Gal 2:10

yao kutoka Kipro na Kirene walikuja Antiokia na kuanza kuongea na watu waliozungumza Kigiriki, wakitangaza habari njema ya Bwana Yesu. **21** Isitoshe, mkono wa Yehova* ulikuwa pamoja nao, na idadi kubwa wakawa waamini na kumgeukia Bwana.^a

22 Kutaniko lililokuwa Yerusalemu likasikia kuwahu-su, nao wakamtuma Barnaba^b mpaka Antiokia. **23** Alipofika na kuziona fadhili zisizostahiliwa za Mungu, akashangilia na kuanza kuwatia moyo wote waendeleo kukaa katika Bwana wakiwa wameazimia moyoni;^c **24** kwa maa-na alikuwa mtu mwema aliyejaa roho takatifu na imani. Na umati mkubwa ukaongezwa kwa Bwana.^d **25** Basi akaenda Tarso kumtafuta Sauli.^e **26** Baada ya kumpata, akamleta Antiokia. Basi kwa mwaka mzima wakakusanyika pamoja nao katika kutaniko na kufundisha umati mkubwa, na huko Antiokia ndiko kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa Wakristo^f kupitia mwongozo wa Mungu.

27 Katika siku hizo manabii^g walishuka kutoka Yerusalemu mpaka Antiokia. **28** Mmoja wao aitwaye Agabo^h akasimama na kutabiri kupitia roho kwamba njaa kubwa ilikuwa karibu kutokea juu ya dunia yote inayokaliwa,ⁱ na kwa kweli ilitokea wakati wa Klaudio. **29** Basi wanafunzi wakaamua kila mmoja kulingana na uwezo wake,^j watume msaada*^k kwa akina ndugu wa-

11:21 *Angalia Nyongeza A5. 11:29 *Au "huduma ya msaada."

lioishi Yudea; **30** nao walifanya hivyo, wakatuma msaada kwa wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli.^a

12 Karibu na wakati huo, Mfalme Herode akaanza kuwatesa baadhi ya watu katika kutaniko.^b **2** Alimua kwa upanga^c Yakobo ndugu ya Yohana.^d **3** Alipoona Wayahudi wamefurahishwa na jambo hilo, akamkamata Petro pia. (Ulikuwa wakati wa Sherehe ya Mikate Isiyu na Chachu.)^e **4** Akamkamata na kumtia gerezani,^f chini ya ulinzi wa zamu nne za wanajeshi wanne kwa kila zamu, naye alikusudia kumtoa* mbele ya watu baada ya Pasaka. **5** Kwa hiyo, Petro alikuwa gerezani lakini kutaniko lilikuwa likisali kwa Mungu kwa bidii sana kwa ajili yake.^g

6 Herode alipokuwa karibu kumtoa, usiku huo Petro alikuwa amelala akiwa amefungwa kwa minyororo miwili katikati ya wanajeshi wawili, na walinzi walikuwa mbele ya mlango wakilinda gereza. **7** Lakini tazama! malaika wa Yehova* alikuwa amesimama hapo,^h na nuru ikang'aa katika chumba cha gereza. Akamgonga Petro ubavuni, akamwamsha akisema: "Simama upesi!" Na minyororo ikaa nguka kutoka kwenye mikonono yake.ⁱ **8** Malaika akamwambia: "Vaa nguo* na uvae viatu vyako." Akafanya hivyo. Mwishowe akamwambia: "Vaa vazi lako la nje, uendelee kunifuata." **9** Naye akatoka na

12:4 *Au "kumtoa ili ahukumiwe."
12:7, 11, 17 *Angalia Nyongeza A5.
12:8 *Au "Jifunge."

SURA YA 11

a Mdo 12:25

SURA YA 12

b Yoh 15:20

c Mt 20:20-23
Lu 11:49

d Mt 4:21

e Kut 12:15
Kut 23:15
Law 23:6

f Lu 21:12

g 2Ko 1:11

h Zb 34:7
Ebr 1:7, 14

i Mdo 5:18, 19

Safu ya 2

a 2Pe 2:9

b Mdo 13:5
Mdo 15:37, 38
Kol 4:10

c Mt 13:55
Mdo 15:13
Mdo 21:18
1Ko 15:7
Gal 1:19
Gal 2:9

kuendelea kumfuata, lakini hakujua kwamba mambo ya liyokuwa yakitendeka kupitia yule malaika yalikuwa halisi. Kwa kweli, alidhani anaona maono. **10** Wakampita mlinzi wa kwanza na wa pili, wakafika kwenye lango la chuma linaloelekea jijini, nalo likafunguka lenyewe mbele yao. Walipotoka nje wakapita kwenye barabara fulani, na mara moja yule malaika akamwachacha. **11** Petro alipotambua kilichokuwa kikitendeka, akasema: "Sasa ninajua kwa hakika kwamba Yehova* alimtuma malaika wake na kunikomboa kutoka mkononi mwa Herode na mambo yote ambayo Wayahudi walitarajia."^a

12 Baada ya kutambua hivyo, akaenda kwenye nyumba ya Maria mama ya Yohana aliyetitwa Marko,^b ambamo watu wengi walikuwa wamekusanyika wakisali. **13** Alipopiga hodi kwenye mlango wa lango kuu, kijakazi anayetitwa Roda akaenda kuangalia. **14** Alipotambua sauti ya Petro, akashangilia sana hivi kwamba badala ya kufungua lango, akarudi ndani mbio na kuwaeleza kwamba Petro amesimama langoni. **15** Wakamwambia: "Umerukwa na akili." Lakini akaendelea kusisitiza kwamba ni kweli. Wakaanza kusema: "Ni malaika wake." **16** Lakini Petro akaendelea kubisha. Walipofungua mlango, wakamwona nao wakashangaa. **17** Lakini akawapungia mkono wanyamaze na kuwambia kirefu jinsi Yehova* alivyomtoa gereza ni, naye akasema: "Waambi ni Yakobo^c na akina ndugu

mambo haya." Ndipo akatoka, akasafiri kwenda mahali pengine.

18 Basi kulipokucha, kuka-wa na mvurugo miongoni mwa wanajeshi kuhusu kili-chompata Petro. **19** Herode akamtafuta kwa bidii, na aliposhindwa kumpata, akawa-hoji walinzi na kuamuru wape-lekwe kuadhibiwa;^a basi akatoka Yudea na kushuka kwenda Kaisaria, akakaa huko kwa muda.

20 Sasa alikuwa amewaka-sirikia* watu wa Tiro na Sidoni. Basi wakaja kwake wakiwa na kusudi moja, na baada ya kumshawishi Bla-sto, mwanamume aliyesimamia nyumba ya mfalme,[#] wakatoa ombi la amani, kwa sababu nchi yao ilipata chakula kutoka kwa nchi ya mfalme. **21** Siku moja iliyochaguliwa, Herode alivaa mavazi ya kifalme akaketi kwenye kiti cha hukumu na kuanza kuwahutubia watu wote. **22** Ndipo watu waliokusanyika wakaanza kusema kwa sauti kubwa: "Hii ni sauti ya mungu, si ya mwanadamu!" **23** Papo hapo, malaika wa Yehova* akampiga, kwa sababu hakumpa Mungu utukufu, naye akaliwa na wadudu akafa.

24 Lakini neno la Yehova* likazidi kukua na kuenea.^b

25 Nao Barnaba^c na Sauli, baada ya kutimiza kikamiliki kazi ya kutoa msaada huko Yerusalemu,^d wakarudi na kumchukua Yohana,^e ambaye pia aliitwa Marko, aende pamoja nao.

12:20 *Au "alitaka kupigana na."
#Tnn., "chumba cha kulala cha mfalme."
12:23, 24; 13:2 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 12

a Mdo 16:27

b Mdo 6:7
Mdo 19:20
Kol 1:6

c Mdo 4:36, 37

d Mdo 11:29, 30

e Mdo 13:5
Mdo 15:37, 38

Safu ya 2

SURA YA 13

a Iko 12:28
Efe 4:11, 12

b Mdo 9:15

c 1Ti 2:7

d Mdo 12:25

13 Basi katika kutaniko la huko Antiokia kulikuwa na manabii na walimu:^a Barnaba, Simioni aliyetitwa Nigeri, Lukio wa Kirene, Manaeni aliyeelimishwa pamoja na Herode mtawala wa wilaya, na Sauli. **2** Walipokuwa wakimhudumia[#] Yehova* na kufunga, roho takatifu ikasema: "Wawekeni kando kwa ajili yangu Barnaba na Sauli^b kwa kazi ambayo nimewaitia."^c **3** Baada ya kufunga na kusali, wakaweka mikono juu yao, na kuwaacha waende.

4 Basi watu hao waliotumwa na roho takatifu, wakashuka kwenda Seleukia, na kutoka huko wakasafiri baharini kwenda Kipro. **5** Walipofika Salami, wakaanza kulingaza neno la Mungu katika masinagogi ya Wayahudi. Pia Yohana alikuwa pamoja nao akiwahudumia.*^d

6 Walipokuwa wamepita katika kisiwa chote mpaka Pafos, wakakutana na mwanamume Myahudi aliyetitwa Bar-Yesu, ambaye alikuwa mlozi na nabii wa uwongo. **7** Alikuwa pamoja na liwali* Sergio Paulo, mwanamume mwenye akili. Akawaita Barnaba na Sauli, kwa kuwa alitamani kulisikia neno la Mungu. **8** Lakini Eli-ma mlozi (kwa maana hivyo ndivyo jina lake lina-vyotafsiriwa) akaanza kuwapinga, akijaribu kumzuia yule liwali asiwe mwamini. **9** Ndipo Sauli, aitwaye pia Paulo, akiwa amejaa roho takatifu, akamtazama kwa makini **10** na

13:2 # Au "wakimhudumia hadharani."
13:5 *Au "akiwasaidia" **13:7** *Gavana Mroma aliyesimamia mkoa. Angalia Kamusi, uku. 2012.

kumwambia: “Ewe mtu uliyepa kila aina ya upunjaji na kila aina ya ulaghai, wewe mwana wa Ibilisi,^a wewe adui wa kila jambo la uadilifu, je, hutaacha kuzipotosha njia za Yehova* zilizo sawa? **11** Tazama! mkono wa Yehova* uko juu yako, nawe utakuwa kipofu, hutaona nuru ya jua kwa kipindi fulani.” Mara moja akaangukiwa na ukungu mzito na giza, naye akazunguka akita-futa mtu wa kumshika mkono ili amwongoze. **12** Yule liwali alipoona jambo lililotokea, akawa mwamini kwa sababu alistaajabishwa na fundisho la Yehova.*

13 Ndipo Paulo na wenzake wakasafiri baharini kutoka Pafo na kufika Perga huko Pamfilia. Lakini Yohana^b akawaacha na kurudi Yerusalemu.^c **14** Hata hivyo, wakae-ndelea na safari kutoka Perga hadi Antiokia huko Pisidia. Nao wakaingia ndani ya sinagogi^d siku ya Sabato, wakaketi. **15** Baada ya kusoma hadharani Sheria^e na Manabii, maofisa wasimamizi wa sinagogi wakawatuma watu kwao, wakisema: “Wanaume, akina ndugu, ikiwa mna neno lolote la kuwatia moyo watu, lisemeni.” **16** Basi Paulo akasimama, akawapungia mkono, akasema:

“Wanaume, Waisraeli nanyi wengine mnaomwogopa Mungu, sikilizeni. **17** Mungu wa watu hawa Israeli aliwachagua mababu zetu, akawainua watu hao walipokuwa wakii-shi wakiwa wageni katika nchi ya Misri na kuwatoa huko kwa mkono ulioinuliwa.^f **18** Na

SURA YA 13

a Yoh 8:44

b Mdo 12:12

c Mdo 15:37, 38

d Mdo 17:1, 2
Mdo 18:4
Mdo 19:8

e Mdo 15:21

f Kut 6:1, 6
Kum 7:6, 8

Safu ya 2

a Kut 16:35
Hes 14:33, 34b Kum 7:1
Yos 14:1, 2c Amu 2:16
1Sa 3:20

d 1Sa 8:4, 5

e 1Sa 10:21
1Sa 11:15f 1Sa 16:12, 13
Zb 89:20

g 1Sa 16:1

h 1Sa 13:13, 14

i 2Sa 7:12
Isa 11:1
Lu 1:31, 32
Lu 1:68, 69

j Mt 3:1, 6

k Mt 3:11
Lu 3:16l Mt 10:5, 6
Lu 24:47, 48

kwa kipindi cha karibu miaka 40, akawavumilia huko nyikani.^a **19** Baada ya kuyaangamiza mataifa saba katika nchi ya Kanaani, akawapa nchi yao iwe urithi wao.^b **20** Hayo yote yalifanyika kwa karibu miaka 450.

“Baada ya hapo akawapa waamuzi hadi wakati wa nabii Samweli.^c **21** Lakini baadaye wakaomba wapewe mfalme,^d na Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi, mwanamume wa kabila la Benjamini,^e kwa miaka 40. **22** Baada ya kumwondoa, akamwinua Daudi awe mfalme wao,^f na akatoa ushahidi kumhusu akisema: ‘Nimempata Daudi mwana wa Yese,^g mtu anayeupendeza moyo wangu;^h atafanya mambo yote ninayotamani.’ **23** Kama alivyoahidi, kutoka katika uzao wa* mwanamume huyu, Mungu amewaletea Israeli mwokozi, yaani, Yesu.ⁱ **24** Kabla ya huyo kufika, Yohana alikuwa amewahubiria hadharani watu wote wa Israeli wabatizwe ili kuonyesha kwamba wametubu.^j **25** Lakini Yohana alipokuwa akimalizia huduma yake, akawa akisema: ‘Mnadhani mimi ni nani? Mimi siye. Lakini tazameni! kuna Mtu anayekuja baada yangu ambaye sistahili kuvifungua viatu vya miguu yake.’^k

26 “Wanaume, akina ndugu, ninyi wazao wa familia ya Abrahamu na wengine kati yenu mnaomwogopa Mungu, neno la wokovu huu limele-twa kwetu.^l **27** Kwa maana wakaaji wa Yerusalemu na watawala wao hawakumtambua

huyo, lakini walipomhukumu walitimiza mambo yaliyosemwa na Manabii,^a ambayo husomwa kwa sauti kila sabato.

28 Ingawa hawakupata sababu ya kumuua,^b walimtaka Pilato aamuru auawe.^c **29** Walipokuwa wametimiza mambo yote yaliyoandikwa kumhusu, walimshusha kutoka kwenye mti na kumlaza kaburini.^{*d} **30** Lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu,^e **31** na kwa siku nyingi akaonekana na wale waliokuwa wameenda naye kutoka Galilaya hadi Yerusalemu. Sasa hao ndio mashahidi wake kwa watu.^f

32 "Basi tunawatangazia habari njema kuhusu ahadi iliyotolewa kwa mababu. **33** Mungu ametimiza kikamili kwetu sisi, watoto wao, kwa kumfufua Yesu;^g kama ilivyoandikwa katika zaburi ya pili: 'Wewe ni mwanangu; leo nimekuwa Baba yako.'^h **34** Na uhakika wa kwamba Yeye alimfufua kutoka kwa wafu ili asirudi tena kwenye uharibifu, Yeye ameutaja kwa njia hii: 'Nitawaonyesha upendo mshikamanifu, ambao ni wa uaminifu,* alioahidiwa Daudi.'ⁱ **35** Pia, zaburi nyingine inasema: 'Hutamruhusu mshikamanifu wako aone uharibifu.'^{*j} **36** Kwa upande wake, Daudi alimtumikia Mungu* katika kizazi chake mwenyewe, akalala usingizi katika kifo, akazikwa pamoja na mababu zake, naye akaona uharibifu.^{*k} **37** Kwa upande mwingine, yule amba-

13:29 *Au "kwenye kaburi la ukumbusho." **13:34** *Au "wenye kutegemeka." **13:35** *Au "aoze." **13:36** *Au "alifanya mapenzi ya Mungu." *Au "na mwili wake ukaoza."

SURA YA 13

a Isa 53:7, 8

b Mt 26:59, 60
Lu 23:13-15
Yoh 19:4c Mt 27:22, 23
Yoh 19:15d Mt 27:59, 60
Yoh 19:40-42e Mt 28:5, 6
Mdo 2:24f Mt 28:16
Mdo 1:3
Mdo 3:15
1Ko 15:4-7

g Ro 1:4

h Zb 2:7
Ebr 1:5
Ebr 5:5

i Isa 55:3

j Zb 16:10
Mdo 2:31

k Mdo 2:29

Safu ya 2

a Mdo 2:27

b Lu 24:46, 47
Mdo 5:31
Mdo 10:43

c Ebr 10:1

d Isa 53:11
Ro 3:28
Ro 5:18
Ro 8:3
Ebr 7:19

e Hab 1:5

f Mdo 11:23
Mdo 14:21, 22g Mdo 14:1, 2
Mdo 17:4, 5h Mt 10:5, 6
Mdo 3:25, 26
Ro 1:16

ye Mungu alimfufua hakuona uharibifu.*^a

38 "Kwa hiyo, acheni iju-likane kwenu, akina ndugu, kwamba kupitia mtu huyo mnatangaziwa msamaha wa dhambi,^b **39** na kwamba mambo yote ambayo hamngatangazwa kuwa bila hatia kulingana na Sheria ya Musa,^c kila mtu anayeamini anatangazwa kuwa bila hatia kupitia mtu huyu.^d **40** Kwa hiyo, jihadharini ili msipatwe na mambo haya yanayosemwa katika Manabii: **41** 'Tazameni, ninyi wenye dharau, na mshangae na kuangamia, kwa sababu ninafanya kazi fulani katika siku zenu, kazi ambayo hamtaiamini kamwe hata mtu yeyote akiwaeleza kirefu.'^{*e}

42 Basi walipokuwa wakiondoka, watu wakawasihi wazungumzie mambo hayo Sabato iliyofuata. **43** Baada ya kusanyiko la sinagogi kumalizika, Wayahudi wengi na wageuzwa imani waliomwabudu Mungu wakawafuata Paulo na Barnaba, ambao walisema nao na kuwahimiza waendeleo kubaki katika fadhili zizozostahiliwa za Mungu.^f

44 Sabato iliyofuata karibu jiji lote lilikusanyika ili kulisi-kia neno la Yehova.* **45** Wayahudi walipouona umati, walijawa na wivu wakaanza kupinga wakikufuru mambo ambayo Paulo alikuwa akisema.^g **46** Kisha Paulo na Barnaba wakawaambia hivi kwa ujasiri: "Ilikuwa lazima neno la Mungu lihubiriwe kwenu kwanza.^h Kwa kuwa mnalika-

13:37 *Au "hakuoza." **13:44** *Angalia Nyongeza A5.

taa na kujiona hamstahili uzima wa milele, tazameni! tunawageukia mataifa.^a **47** Kwa maana Yehova* ametuamuru kwa maneno haya: 'Nimewachagua muwe nuru ya mataifa, na muwe wokovu mpaka miisho ya dunia.'^b

48 Watu wa mataifa waliposikia jambo hilo, wakaanza kushangilia na kulitukuza neno la Yehova,* na wote waliokuwa na mwelekeo unaofaa kwa ajili ya uzima wa milele wakawa waamini. **49** Zaidi ya hayo, neno la Yehova* lilikuwa likienezwa katika nchi yote. **50** Lakini Wayahudi wakawachochea wanawake mashuhuri waliomwogopa Mungu, na wakuu wa jiji, nao wakaanza kwatesa^c Paulo na Barnaba na kuwatupa nje ya mipaka yao. **51** Basi wakawakung'utia mavumbi yaliyokuwa kwenye miguu yao na kwenda Ikoniamu.^d **52** Nao wanafunzi wakaendelea kujawa na shangwe^e na roho takatifu.

14 Basi huko Ikoniamu wakaingia pamoja katika sinagogi la Wayahudi, wakazungumza vizuri hivi kwamba umati mkubwa wa Wayahudi na pia Wagiriki wakawa waamini. **2** Lakini Wayahudi ambao hawakuamini wakawachochea watu* wa mataifa na kuwafanya wawachukie akina ndugu.^f **3** Basi wakatamia muda mrefu wakizungumza kwa ujasiri kwa mamlaka ya Yehova,* aliyetoa ushahidi kuhusu neno la fadhili zake zisizostahiliwa kwa kuwaruhusu wafa-

13:47-49; 14:3 *Angalia Nyongeza A5. 14:2 *Au "nafsi za watu."

SURA YA 13

a Lu 2:29-32
Mdo 18:5, 6
Ro 10:19

b Isa 49:6
Mdo 1:8

c Mt 23:34
Mdo 14:2, 19
Mdo 17:5

d Mt 10:14
Lu 9:5

e Mt 5:12

SURA YA 14

f Mdo 13:45

Safu ya 2

a Mdo 19:11
Ebr 2:3, 4

b Mdo 14:19

c Mt 10:23

d Mt 9:28

e Isa 35:6

f Mdo 28:3-6

nye ishara na mambo ya aja-bu.*^a **4** Hata hivyo, umati wa jiji ulikuwa umegawanyika; baadhi yao walikuwa upande wa Wayahudi lakini wengine upande wa mitume. **5** Watu wa mataifa na Wayahudi, pamoja na watawala wao walipojaribu kuwatendea kwa dhara-rau na kuwapiga mawe,^b **6** wakajulishwa jambo hilo, nao wakakimbilia majiji ya Likaoonia, Listra na Derbe, na maeneo yaliyokuwa karibu.^c **7** Wakiwa huko, wakaendelea kutangaza habari njema.

8 Huko Listra, kulikuwa na mwanamume aliyekuwa ameteki akiwa amelemaa miguu. Alikuwa kiwete tangu kuzaliwa na hakuwa ametembea kamwe. **9** Mtu huyo alikuwa akimsikiliza Paulo alipokuwa akizungumza. Paulo alipomtazama kwa makini na kuona kwamba ana imani ya kuponywa,^d **10** akasema kwa sauti kubwa: "Simaan kwa miguu yako." Ndipo yule mwanamume akaruka na kuanza kutembea.^e **11** Umati ulipoona jambo alilofanya Paulo, wakasema kwa sauti kubwa katika lugha ya Kili-kaonia: "Miungu imekuwa kama wanadamu nayo imeshuka kwetu!"^f **12** Wakaanza kumwita Barnaba Zeu, naye Paulo wakamwita Herme, kwa kuwa ndiye aliyeeongoza katika mazungumzo. **13** Naye kuhani wa Zeu, ambaye hekalu lake lilikuwa kwenye mwingilio wa jiji, akawaleta ng'ombe dume na mashada ya maua kwenye malango, naye alitaka kutoa dhabihu pamoja na umati.

14:3 *Au "miujiza."

14 Hata hivyo, mitume Barnaba na Paulo waliposikia jambo hilo, wakayararua mavazi yao na kuruka ndani ya umati wakisema kwa sauti kubwa: **15** "Wanaume, kwa nini mnafanya mambo haya? Sisi pia ni wanadamu tulio na udhaifu kama wenu.^a Nasi tunawatangazia habari njema, ili mgeuke kutoka katika mambo haya ya bure mje kwa Mungu aliye hai, aliyumba mbingu na dunia na bahari na vitu vyote vilivyomo.^b **16** Katika vizazi vilivyopita aliruhusu watu wa mataifa yote waendeleo kutembea katika njia zao,^c **17** ingawa hakujiacha bila ushahidi^d kwa kuwa alitenda mema, akiwapa ninyi mvua kutoka mbinguni na majira ya mavuno,^e akiwashibisha kwa chakula na kuijaza mioyo yenu furaha."^f **18** Na ingawa walisema mambo hayo, haikuwa rahisi kwao kuuzuia umati kuwatolea dhabihu.

19 Lakini Wayahudi wakafika kutoka Antiokia na Ikoniamu wakaushawishi umati,^g nao wakampiga Paulo kwa mawe na kumkokota nje ya jiji, wakiwazia kwamba amekufa.^h **20** Hata hivyo, wanafunzi walipomzunguka, akasimama na kuingia jijini. Siku iliyofuata akaondoka pamoja na Barnaba kwenda Derbe.ⁱ **21** Baada ya kulitangazia jiji hilo habari njema na kuwafanyia watu wengi kuwa wanafunzi, wakarudi Lистра, Ikoniamu, na Antiokia. **22** Wakiwa huko wakawatia nguvu wanafunzi*^j na kuwatia moyo wabaki katika imani wakisema:

14:22 *Au "wakazitia nguvu nafsi za wanafunzi."

SURA YA 14

a Mdo 10:25, 26

b Kut 20:11
Zb 146:6

c Mdo 17:30

d Mdo 17:26, 27
Ro 1:20e Zb 147:8
Yer 5:24
Mt 5:45

f Zb 145:16

g Mdo 17:13

h 2Ko 11:25

i Mdo 16:1

j Mdo 11:22, 23

Safu ya 2

a Mt 10:38
Yoh 15:19
Ro 8:17
1Th 3:4

b Tit 1:5

c Mdo 13:2, 3

d Mdo 13:13

e Mdo 13:1, 2

f Mdo 11:18

SURA YA 15

g Mwa 17:9, 10
Kut 12:48
Law 12:2, 3

h Gal 2:1

"Ni lazima tuingie katika Ufalme wa Mungu kupitia dhiki nyingi."^a **23** Isitoshe, wakaweka rasmi wazee kwa ajili yao katika kila kutaniko,^b wakatoa sala na kufunga,^c nao wakawakabidhi kwa Yehova* ambaye walikuwa wamemwamini.

24 Kisha wakapitia Pisidia wakaingia Pamfilia,^d **25** na baada ya kulitangaza neno huko Perga, wakashuka kwenda Atalia. **26** Kutoka huko wakasafiri baharini kwenda Antiokia, ambako walikuwa wamekabidhiwa kwenye fadhili zisizostahiliwa za Mungu kwa ajili ya kazi ambayo sasa walikuwa wamemaliza.^e

27 Walipofika na kulikusanya kutaniko pamoja, wakawasimulia mambo mengi ambayo Mungu alikuwa amefanya kupitia kwao, na kwamba alikuwa amewafungulia mataifa mlango wa kuingia kwenye imani.^f **28** Basi wakakaa pamoja na wanafunzi kwa muda mrefu.

15 Sasa watu fulani wakashuka kutoka Yudea na kuanza kuwafundisha akina ndugu: "Msipotahiriwa kulingana na desturi ya Musa,^g hamwezi kuokolewa." **2** Baada ya Paulo na Barnaba kutolewana na kubishana sana na watu hao, wakapanga Paulo na Barnaba na wengine wapande kwenda kwa mitume na wazee huko Yerusalem^h kuuiliza kuhusu jambo* hilo.

3 Basi, baada ya kusindikizwa umbali fulani na kutaniko, watu hao wakaenda waka-

14:23 *Angalia Nyongeza A5. 15:2 *Au "bishano."

pitia Foinike na Samaria, wakisimulia kirefu kuhusu ku-geuka kwa watu wa mataifa, nao wakafanya akina ndugu washangilie sana. **4** Walipofika Yerusalemu, walikaribishwa kwa fadhili na kutaniko na mitume na wazee, nao wakawasimulia mambo mengi ambayo Mungu alifanya kupitia kwao. **5** Lakini baadhi ya wale wa madhehebu ya Mafarisayo ambao sasa walikuwa waamini wakasimama kutoka kwenye viti vyao na kusema: “Ni lazima watahiriwe na kuwaamuru washike Sheria ya Musa.”^a

6 Basi, mitume na wazee wakakusanyika pamoja ili kulichunguza jambo hilo. **7** Baada ya kujadiliana sana, *Petro akasimama na kuwaambia: “Wanaume, akina ndugu, mnajua vema kwamba tangu siku za zamani Mungu alinichagua kati yenu ili kupitia kinywa changu watu wa mataifa wasikie neno la habari njema na kuamini.”^b **8** Pia, Mungu anayejua moyo,^c alitoa ushahidi kwa kuwapa roho takatifu,^d kama vile alivyotupatia sisi. **9** Naye hakutofautisha hata kidogo kati yetu na wao,^e bali alisafisha mioyo yao kwa imani.^f **10** Basi kwa nini sasa mnamjaribu Mungu kwa kuweka kwenye shingo za wanafunzi nira^g ambayo mababu zetu na sisi wenyewe tulishindwa kuibeba?^h **11** Badala yake, sisi tunaamini kwamba tunaokolewa kupitia fadhili zisizostahiliwa za Bwana Yesuⁱ katika njia ileile wanayookolewa.”^j

15:7 *Au “kubishana sana.”

SURA YA 15

a Kut 12:48
Mdo 11:2, 3

b Mdo 10:34, 35
Mdo 11:16, 17

c 1Nya 28:9
Yer 11:20

d Mdo 10:44, 45
Mdo 11:15

e Gal 3:28

f Gal 2:15, 16
1Pe 1:22

g Gal 5:1

h Gal 3:10

i Isa 53:11
Yoh 1:17

j Mt 20:28

Safu ya 2

a Mt 10:2
Mdo 11:13
2Pe 1:1

b 1Pe 2:9, 10

c Amo 9:11, 12

d Isa 45:21

e Mdo 15:10

f Mwa 35:2
Kut 20:3
1Ko 10:14

g 1Ko 6:9, 10
Kol 3:5
1Th 4:3

h Mwa 9:4
Law 3:17
Law 7:26
Law 17:10, 13
Law 19:26
Kum 12:23
Kum 15:23
1Sa 14:32, 33

12 Ndipo kikundi chote kikanyamaza na kuanza kuwasikiliza Barnaba na Paulo wakisimulia ishara nyingi na mambo ya ajabu* ambayo Mungu alifanya kupitia kwao miongoni mwa mataifa. **13** Walipomaliza kuzungumza, Yakobo akasema: “Wanaume, akina ndugu, nisikilizeni. **14** Simioni^a amesimulia kikamili jinsi Mungu kwa mara ya kwanza alivyoelekeza uangalifu wake kwa mataifa ili achukue kutoka kwao watu kwa ajili ya jina lake.”^b **15** Na maneno ya Manabii yanauunga mkono jambo hilo, kama ilivyoandikwa: **16** ‘Baada ya mambo hayo nitarudi na kuliihua tena hema la* Daudi ambalo limeanguka chini; nitayajenga upya magofu yake na kulirudisha tena, **17** ili watu wanaobaki wamtafute Yehova* kwa bidii, pamoja na watu wa mataifa yote, watu wanaoitwa kwa jina langu, asema Yehova,* anayefanya mambo haya,^c **18** yanayojulikana tangu zamani.’^d **19** Kwa hiyo uamuzi wangu* ni kutowataabisha watu wa mataifa wanaomgeukia Mungu,^e **20** bali kuwaandikia wajiepushe na vitu vilivyochafuliwa na sanamu,^f na uasherati,^g na vitu vilivyonyongwa,^h na damu.^h **21** Kwa maana tangu nyakati za kale kuna watu ambao wamekuwa wakihubiri kumhusu Musa katika kila jiji, kwa sababu yeye

15:12 *Au “miujiza.” 15:16 *Au “kibanda cha; nyumba ya.” 15:17 *Angalia Nyongeza A5. 15:19 *Au “maoni yangu.” 15:20 *Neno la Kigiriki *pornei*^a. Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au “wanayama walioauwa bila kutolewa damu.”

husomwa kwa sauti kubwa katika masinagogi kila sabato.”^a

22 Ndipo mitume na wazee, pamoja na kutaniko lote wa-kaamua kuwatuma wanaume waliochaguliwa kutoka miongoni mwao waende Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba; waliwatuma Yuda aliyeitwa Barsaba, na Sila,^b wanaume waliokuwa wakiongoza kati ya akina ndugu. **23** Wakaandika maneno haya na ku-yatuma kupitia kwao:

“Mitume na wazee, ndugu zenu, kwa ndugu walio huko Antiokia,^c Siria, na Kilikia ambao ni wa kutoka kwa mataifa: Salamu! **24** Kwa kuwa tumesikia kwamba watu fulani walitoka miongoni mwenu na kuwataabisha kwa mambo waliyosema,^d wakijaribu kuwawuruga,* ingawa hatukuwapa maagizo yoyote, **25** tumefikia kauli moja kwamba tuwachague wanaume ili tuwatume kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo, **26** wanaume ambao wametoa uhai wao* kwa ajili ya jina la Bwana wetu Yesu Kristo.^e **27** Kwa hiyo, tunawatuma Yuda na Sila, ili wao pia waeleze mambo hayohayo kwa maneno.^f **28** Kwa maana roho takatifu^g na sisi wenyewe tumeona ni vizuri tusiwaongeze ninyi mzungu zaidi ila mambo haya ya lazima: **29** kuendelea kujiepusha na vitu vilivyotolewa dhahabu kwa sanamu,^h na damu,ⁱ na vitu vilivyonyongwa,^{*j} na uasherati.^{#k} Mkijiepusha kwa ua-

15:24 *Au “kuzivuruga nafsi zenu.” 15:26 *Au “nafsi zao.” 15:29 *Au “wanyama waliouawa bila kutolewa damu.” #Neno la Kigiriki *pornei*’a. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 15

a Mdo 13:15
2Ko 3:15

b 1Th 1:1
1Pe 5:12

c Mdo 11:26

d Mdo 15:1

e Mdo 13:50
1Ko 15:30, 31
2Ko 11:23-26

f Mdo 16:4

g Yoh 16:13
Mdo 5:32

h Mwa 35:2
Kut 20:3
Kut 34:15
1Ko 10:14

i Mwa 9:4
Law 3:17
Law 7:26
Law 17:10
Kum 12:16, 23
1Sa 14:32, 33

j Law 17:13

k Mwa 39:7-9
1Ko 6:9, 10
Efe 5:5
Kol 3:5
1Th 4:3

Safu ya 2

a Mdo 18:23

b 2Ko 11:28

c Mdo 13:4, 5
Kol 4:10
2Ti 4:11

d Mdo 13:13

e Mdo 4:36, 37

ngalifu na mambo haya, mtafanikiwa. Afya njema kwenu!”*

30 Basi, watu hao walipoondoka wakashuka kwenda Antiokia, nao wakakusanya kundi lote pamoja na kuwapa barua hiyo. **31** Baada ya kuisoma, wakashangilia kwa sababu ya kutiwa moyo. **32** Nao Yuda na Sila, kwa sababu walikuwa manabii pia, wakawatia moyo aki-na ndugu kwa hotuba nyingi na kuwaimarisha.^a **33** Baada ya kukaa huko kwa muda fulani, ndugu hao wakawaacha warudi kwa amani kwa wale waliokuwa wame-watuma. **34** *— **35** Lakini Paulo na Barnaba wakakaa Antiokia, wakifundisha na kutangaza habari njema ya neno la Yehova,* wakiwa pamoja na wengine wengi.

36 Baada ya siku kadhaa, Paulo akamwambia Barnaba: “Turudi[#] tukawatembelee aki-na ndugu katika kila jiji ambalo tulitangaza neno la Yehova* tuone jinsi wanavyoendelea.”^b **37** Barnaba alikuwa amezimiza kwenda na Yohana, aliyeitwa Marko.^c **38** Lakini Paulo hakutaka waende pamoja naye, kwa sababu alikuwa amewaacha huko Pamfilia na hakuenda pamoja nao kwenye kazi.^d **39** Ndipo wakagombana kwa ukali hivi kwamba wakaachana; naye Barnaba^e akamchukua Marko na kusafiri pamoja naye baharini kwenda Kipro. **40** Paulo akamchagua Sila na kuondoka baada ya akina ndugu kumka-

15:29 *Au “Kwaherini.” 15:34 *Angalia Nyongeza A3. 15:35, 36 *Angalia Nyongeza A5. 15:36 #Au labda, “Kwa vyoyote vile turudi.”

bidhi kwenye fadhili zisizostahiliwa za Yehova.*^a **41** Akapitia Siria na Kilikia, akiyamrisha makutaniko.

16 Kwa hiyo akafika Derbe na pia Listra.^b Huko kulikuwa na mwanafunzi aliyemitwa Timotheo,^c mama yake alikuwa Myahudi aliyekuwa mwamini, lakini baba yake alikuwa Mgriki, **2** na alishuhudiwa vema na akina ndugu huko Listra na Ikoniamu. **3** Paulo alitamani Timotheo aende pamoja naye, basi akamchukua na kumtahiri kwa sababu ya Wayahudi waliokuwa katika sehemu hizo,^d kwa maana wote walijua kwamba baba yake ni Mgriki. **4** Walipokuwa wakipita katika majiji, walikuwa wakiwapa maagizo yaliyokuwa yameamuliwa na mitume na wazee waliokuwa Yerusalemu ili wayahike.^e **5** Ndipo kwa kweli makutaniko yakaendelea kumrisha katika imani na kuongezeka idadi siku baada ya siku.

6 Zaidi ya hayo, wakapitia Frigia na nchi ya Galatia,^f kwa sababu roho takatifu iliwakataza kuhubiri lile neno katika mkoa wa Asia. **7** Vilevile, walipofika Misia wakajaribu kuingia Bithinia,^g lakini roho ya Yesu haikuwaruhusu. **8** Basi wakapita* Misia na kushuka mpaka Troa. **9** Naye Paulo akaona maono usiku—mwanamume Mmakedonia alikuwa amesimama hapo aki-
msihi: “Vuka uingie Makedonia utusaidie.” **10** Mara tu alipoona maono hayo, tukajaribu kuingia Makedonia, tuki-

15:40; 16:14, 15 * Angalia Nyongeza A5. 16:8 * Au “wakapitia.”

SURA YA 15

a Mdo 14:26

SURA YA 16

b Mdo 14:5-7
ZTi 3:11

c Mdo 19:22
Ro 16:21
IKo 4:17
1Th 3:2
1Ti 1:2

d IKo 9:20

e Mdo 15:28, 29

f Mdo 18:23

g 1Pe 1:1

Safu ya 2

a Flp 1:1

b Ufu 1:11

c Mdo 16:33
Mdo 18:8

d Law 19:31
Law 20:6

e Mk 1:23, 24
Lu 4:41

kata kauli kwamba Mungu alikuwa ametuita tuwatangazie habari njema.

11 Basi tukatoka Troa na kusafiri moja kwa moja baharini hadi Samothrake, lakini kesho yake tukafika Neapoli; **12** na kutoka huko tukaenda Filipi,^a koloni ambalo ni jiji kuu la wilaya ya Makedonia. Tukakaa katika jiji hilo siku kadhaa. **13** Siku ya Sabato tukatoka nje ya lango kando ya mto, ambako tulifikiri kuna mahali pa sala, tuka-
keti na kuanza kuzungumza na wanawake waliokuwa wamekusanyika. **14** Na mwana-
mke aliyeitwa Lidia, muuzaji wa nguo za rangi ya zambaurau, wa jiji la Thiatira^b aliyekuwa mwabudu wa Mungu, alikuwa akisikiliza, na Yehova* akaufungua moyo wake wazi ili asikilize kwa makini mambo ambayo Paulo alikuwa akisema. **15** Basi yeye na watu wa nyumbani mwake walipobatizwa,^c akatusihi: “Ikiwa mmeniona kuwa mwamini-
fu kwa Yehova,* njooni mkae nyumbani kwangu.” Naye akatuhimiza sana twende.

16 Ikatukia kwamba tulipo-
kuwa tukienda mahali pale pa kusali, tulikutana na kijakazi fulani mwenye roho, roho mwovu wa uaguzi.^d Aliwapatia mabwana zake faida nyingi kwa kubashiri.* **17** Msi-
chana huyo alikuwa aki-
mfuata Paulo na sisi akisema kwa sauti kubwa: “Watu hawa ni watumwa wa Mungu Aliye Juu Zaidi^e nao wanawatangazia ninyi njia ya wokovu.” **18** Akaendelea kufanya hivyo kwa siku nyingi. Mwishowe

16:16 * Au “kupiga ramli.”

Paulo akachoshwa, akageuka na kumwambia huyo roho: "Ninakuamuru katika jina la Yesu Kristo umtoke." Naye akatoka saa hiyohiyo.^a

19 Basi, mabwana zake walipoona kwamba wamepoteza tumaini lao la kupata faida,^b wakawakamata Paulo na Sila wakawakokota hadi sokoni kwa watawala.^c **20** Wakawapeleka kwa mahakimu wa raia, na kusema: "Watu hawa wanasumbua sana jiji letu.^d Wao ni Wayahudi, **21** nao wanatangaza desturi ambazo si halali kwetu kuzikubali au kuzifuata, kwa kuwa sisi ni Waroma." **22** Umati ukasimama pamoja dhidi yao, nao wale mahakimu wa raia, baada ya kuyararua mavazi yao, wakaamuru wapigwe kwa fimbo.^e **23** Baada ya kuwapiga sana, wakawatupa gerezani na kumwagiza mlinzi wa jela awalinde.^f **24** Kwa sababu alipewa agizo hilo, akawatupa katika gereza la ndani zaidi na kuifunga miguu yao katika mikatale.

25 Lakini karibu katikati ya usiku, Paulo na Sila walikuwa wakisali na kumsifu Mungu kwa wimbo,^g nao wafungwa walikuwa wakiwasikiliza. **26** Ghafila tetemeko kubwa la ardhi likatokea na misingi ya jela ikatikiswa. Isitoshe, milango yote ikafunguliwa mara moja, na vifungo vyao wote vikafunguka.^h **27** Mlinzi wa jela alipoamka na kuona milango ya gereza imefunguka, akauchomoa upanga wake naye karibu ajiue, akidhani wafungwa walikuwa wametoroka.ⁱ **28** Lakini Paulo akamwambia kwa sauti kubwa: "Usi-

SURA YA 16

a Mt 17:18
Mk 1:25, 26
Mk 1:34
Lu 9:1
Lu 10:17

b Mdo 19:24, 25

c Mt 10:18

d Mdo 17:6

e 1Th 2:2

f Lu 21:12

g Efe 5:19
Kol 3:16

h Mdo 5:18-20
Mdo 12:7

i Mdo 12:18, 19

Safu ya 2

a Yoh 3:16
Yoh 6:47

b Mdo 8:12

c Mdo 22:25
Mdo 23:27

jiimize, kwa maana sisi sote tupo hapa!" **29** Kwa hiyo akaomba taa akakimbia ndani, akitetemeka, akaanguka chini mbele ya Paulo na Sila. **30** Akawaleta nje na kusema: "Mabwana zangu, nifanye nini ili niokolewe?" **31** Wakajibu: "Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokolewa, wewe na watu wa nyumba yako."^a **32** Nao wakamhubiria neno la Yehova* yeye pamoja na wote waliokuwa katika nyumba yake. **33** Naye akawachukua saa hiyo ya usiku, akaosha vido-nda vyao. Kisha yeye na watu wote wa nyumba yake wakabatizwa bila kukawia.^b **34** Akawaleta nyumbani kwake akaandaa meza mbele yao, naye akashangilia sana pamoja na watu wote wa nyumba yake kwa kuwa sasa alikuwa amemwamini Mungu.

35 Ilipofika mchana, mahakimu wa raia wakawatuma maofisa wa polisi wakaseme: "Wafungueni wale watu." **36** Mlinzi wa jela akamweleza Paulo maneno yao: "Mahakimu wa raia wamewatuma watu ili ninyi wawili mfunguliwe. Basi tokeni sasa mwen-nde zenu kwa amani." **37** Lakini Paulo akawaambia: "Walitupiga viboko hadharani bila kutuhukumu,* ingawa sisi ni Waroma,^c na wakatutupa gerezani. Je, sasa wanatufukuza kwa siri? Hapana, haiwezekani! Acha waje watutoe nje wao wenyewe." **38** Wale maofisa wa polisi wakawaeleza mahakimu wa raia maneno hayo. Nao wakaogopa waliposikia kwamba watu hao walikuwa

16:32 *Angalia Nyongeza A5. 16:37

*Au "bila uamuzi wa mahakama."

Waroma.^a **39** Basi wakaja na kuwasihhi na baada ya kuwatoa nje, wakawaomba waondoke katika jiji hilo. **40** Lakini wakatoka gerezani na kwenda nyumbani kwa Lidia; na walipowaona akina ndugu, wakawatia moyo^b kisha wakaoondoka.

17 Sasa wakasafiri kupitia Amfipoli na Apolonia wakaenda hadi Thesalonike,^c ambako kulikuwa na sinagogi la Wayahudi. **2** Basi kulingana na desturi ya Paulo^d akaingia ndani ya sinagogi, na kwa sabato tatu akajadiliana nao akitumia Maandiko,^e **3** akieleza na kuthibitisha kwa marejeo kwamba ilikuwa lazima Kristo atesekke^f na kufufuliwa kutoka kwa wafu,^g akisema: “Huyu ndiye Kristo, Yesu huyu ninayewatangazia ninyi.” **4** Kwa hiyo, baadhi yao wakaamini na kujiunga na Paulo na Sila,^h pia umati mkubwa wa Wagiriki waliomwabudu Mungu, vilevile wanawake wengi mashuhuri.

5 Lakini Wayahudi wakawa na wivu,ⁱ wakakusanya wanaume fulani waovu waliokuwa wakizurura sokoni, wakafanyiza kikundi chenye ghasia kisha wakazusha fujo jijini. Wakaishambulia nyumba ya Yasoni wakitaka Paulo na Sila waletwe nje kwenye kile kikundi. **6** Walipowakosa wakamkokota Yasoni na baadhi ya akina ndugu mpaka kwa watawala wa jiji, wakisema kwa sauti kubwa: “Watu hawa ambao wameipindua* dunia inayokaliwa wako hapa pia,^j **7** naye Yasoni amewa-

17:6 *Au “wameleta vurugu katika.”

SURA YA 16

a Mdo 22:27-29

b 2Ko 1:3, 4

SURA YA 17

c 1Th 2:1

d Mdo 9:19, 20

Mdo 13:13, 14

Mdo 14:1

Mdo 18:4

e Mdo 18:19

f Zb 22:7

Zb 34:20

Zb 69:21

Zb 118:22

Isa 50:6

Isa 53:3, 5

g Zb 16:10

Lu 24:45, 46

h Mdo 15:22, 40

i Mdo 13:45

j Mdo 16:19-21

Safu ya 2

a Lu 23:1, 2

Yoh 19:12

b Mdo 14:2, 19

c Mt 10:23

d Mdo 16:1, 2

1Th 3:2

karibisha. Watu hao wote wanapinga maagizo ya Kaisari, wakisema kuna mfalme mwingine, Yesu.”^a **8** Ule umati na watawala wa jiji waliposikia mambo hayo, wakashtuka; **9** baada ya kuchukua dhamaana ya kutosha kutoka kwa Yasoni na wale wengine, wakawaacha waende zao.

10 Mara tu ilipofika usiku, akina ndugu wakawatuma Paulo na Sila waende Beroya. Walipofika huko, wakaingia ndani ya sinagogi la Wayahudi. **11** Sasa watu hawa walikuwa wasikivu kuliko wale wa Thesalonike, kwa maana walilikubali neno kwa hamu kubwa ya akili, wakiyachunguza Maandiko kwa uangalifu kila siku ili kuona kama mambo hayo ndivyo yalivyo. **12** Kwa hiyo wengi wao wakawa waamini, vilevile wanawake wengi Wagiriki walioheshimiwa na pia baadhi ya wanaume. **13** Lakini Wayahudi kutoka Thesalonike waliposikia kwamba Paulo alikuwa akitangaza pia neno la Mungu huko Beroya, wakaja huko ili kuchochea na kuuvuruga umati.^b **14** Mara moja akina ndugu wakamsindikiza Paulo mpaka baharini,^c lakini Sila na Timotheo wakabaki huko. **15** Hata hivyo, wale waliomsindikiza Paulo wakaenda naye mpaka Athene, kisha wakarudi baada ya kupokea maagizo kwamba Sila na Timotheo^d wamfuata Paulo haraka iwezekanavyo.

16 Paulo alipokuwa akiwasubiri huko Athene, roho yake ikaudhika sana alipoona kwamba jiji hilo lilikuwa limejaa sanamu. **17** Basi akaanza kujadiliana katika sinagogi

pamoja na Wayahudi na watu wengine waliomwabudu Mungu na kila siku pamoja na watu aliowakuta sokoni.

18 Lakini baadhi ya Waepikurea na wanafalsafa Wastoa wakaanza kubishana naye, wengine wao wakisema: “Mpi-gadomo huyu anataka kusema nini?” Nao wengine: “Inaonekana anatangaza miungu ya kigeni.” Kwa sababu alikuwa akihubiri habari njema ya Yesu na ufufuo.^a **19** Kwa hiyo wakamshika na kumpeleka Areopago, wakisema: “Je, tunaweza kujua ni fundisho gani hili jipya unalozungumzia? **20** Kwa maana unaanzisha mambo yaliyo mageni masikioni mwetu, na tunataka kujua yanamaanisha nini.” **21** Kwa kweli, Waathene wote na wageni waliokaa* huko walitumia muda wao wa starehe bila kufanya kitu kingine isipokuwa kuambiana au kusikiliza jambo jipya. **22** Basi Paulo akasimama katikati ya Areopago^b na kusema:

“Wanaume wa Athene, ni-naona kwamba katika mambo yote mnaonekana kuwa mnaogopa sana miungu* kuliko watu wengine.^c **23** Kwa mfanano, nilipokuwa nikipita na kutazama kwa uangalifu vitu vyenu vya ibada, niliona pia madhabahu iliyoandikwa, ‘Kwa Mungu Asiyejulikana.’ Kwa hiyo, kile mnachobudu bila kujua, hicho ndicho ninachowatangazia. **24** Mungu aliyeumba ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, akiwa, kama alivyo, Bwana wa mbingu na dunia,^d hakai ka-

17:21 *Au “waliotembelea.” 17:22 *Au “mnapenda sana dini.”

SURA YA 17

a Yoh 5:28, 29
Yoh 11:25
1Ko 15:12

b Mdo 17:33, 34

c Mdo 17:16

d Zb 146:6

Safu ya 2

a 1Fa 8:27

b Zb 50:12

c Isa 42:5

d Mwa 5:2

e Mwa 1:28

f Kum 2:5, 19
Kum 32:8
Zb 74:17

g Kum 4:29
Zb 145:18
Ro 1:20

h Mwa 1:27

i Kum 5:8
Isa 37:19
Isa 40:18-20
Isa 46:5

j Efe 4:17, 18

k Zb 96:13
Zb 98:9
Yoh 5:22
Mdo 10:42

l Yoh 11:25
Mdo 2:24
Mdo 13:32, 33

m 1Ko 1:23

tika mahekalu yaliyotengenezwa kwa mikono;^a **25** wala hatumikiwi kwa mikono ya binadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote,^b kwa sababu yeye mwenyewe huwapa watu wote uhai na pumzi^c na vitu vyote. **26** Naye alifanyiza kila taifa la watu kutoka kwa mtu mmoja^d ili wakae juu ya uso wa dunia nzima,^e na akaamuru nyakati na kuweka mipaka ya makao ya watu,^f **27** ili wamtafute Mungu, ikiwa watapapasa-papasa wakimtafuta na kwa kweli wampate,^g ingawa, kwa hakika, hayuko mbali na kila mmoja wote. **28** Kwa maana kupitia kwake tuko hai, tunatembea, na tunaishi, hata kama vile ambavyo baadhi ya washairi wenu wamesema, ‘Kwa maana sisi pia ni watoto* wake.’

29 “Kwa hiyo, kwa kuwa sisi ni watoto* wa Mungu,^h hatupaswi kufikiri kwamba Mungu ni kama dhahabu au fedha au jiwe, kama kitu kilichocho-ngwa kwa ufundi na ubunifu wa wanadamu.ⁱ **30** Ni kweli, Mungu ameachilia nyakati hizo za kutojua;^j lakini sasa anawatangazia wanadamu wote kila mahali kwamba wanapaswa kutubu. **31** Kwa sababu ameweka siku ambayo anakusudia kuihukumu^k kwa uadilifu dunia inayokaliwa kupitia mwanamume ambaye amemweka rasmi, naye ametoa uhakikisho kamili kwa watu wote kwa kuwa amemfufua kutoka kwa wafu.”^l

32 Sasa waliposikia kuhusu ufufuo wa wafu, baadhi yao wakaanza kumdhihaki,^m huku wengine wakisema: “Tutaku-

17:28, 29 *Au “uzao.”

sikiliza kuhusu jambo hili wakati mwingine.” **33** Basi Paulo akawaacha, **34** lakini wanaume fulani wakajiunga naye na kuwa waamini. Miongoni mwao kulikuwa na Dionisio, aliyekuwa mwamuzi wa mahakama ya Areopago, na mwanamke aliyelitwa Damari, na wengineo.

18 Baada ya hayo, akatoka Athene na kwenda Korintho. **2** Naye akamkuta Myahudi aliyelitwa Akila,^a mzaliwa wa Ponto aliyekuwa amekuja hivi karibuni kutoka Italia na Prisila mke wake, kwa sababu Klaudio alikuwa ameagiza Wayahudi wote waondoke Roma. Basi akaenda kwao, **3** na kwa sababu walifanya kazi ileile, akakaa nyumbani kwao na kufanya kazi pamoja nao,^b kwa maana kazi yao ilikuwa ya kutengeneza mahema. **4** Alikuwa akitoa hotuba* katika sinagogi^c kila sabato^d na kuwashawishi Wayahudi na Wagiriki.

5 Basi, Sila^e na Timotheo^f waliposhuka kutoka Makedonia, Paulo akaanza kushughulika sana na lile neno, akiwatolea Wayahudi ushahidi ili kuthibitisha kwamba Yesu ndiye Kristo.^g **6** Lakini walipoendelea kumpinga na kumtukana, akayakung'uta mavazi yake^h na kuwaambia: “Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu wenyewe.ⁱ Mimi ni safi.^j Kuanzia sasa nitaeenda kwa watu wa mataifa.”^k **7** Basi akatoka humo* na kuingia katika nyumba ya mwanamume aliyelitwa Titio Yusto, mwabudu wa Mungu, amba-

18:4 *Au “Alikuwa akijadiliana nao.”
18:7 *Yaani, sinagogi.

SURA YA 18

a Mdo 18:24, 26
1Ko 16:19
2Ti 4:19

b Mdo 20:34
1Ko 4:11, 12
1Ko 9:15
1Th 2:9
2Th 3:8, 10

c Mt 4:23

d Mdo 17:2

e Mdo 15:27
Mdo 17:14

f Mdo 16:1, 2
1Th 3:6

g Mdo 17:2, 3
Mdo 28:23

h Mt 10:14

i Eze 33:4

j Mdo 20:26

k Mdo 13:46
Mdo 28:28
Ro 1:16

Safu ya 2

a 1Ko 1:14

b Mt 28:20

c Mdo 23:29
Mdo 25:19

d 1Ko 1:1

ye nyumba yake ilikuwa ime-shikana na sinagogi. **8** Lakini Krispo,^a ofisa msimamizi wa sinagogi akamwamini Bwana, yeye pamoja na watu wote wa nyumba yake. Na Wakorintho wengi waliosikia wakaa-nza kuamini na kubatizwa. **9** Isitoshe, Bwana akamwambia Paulo katika maono usiku: “Usiogohe, bali endelea kusema na usinyamaze, **10** kwa sababu niko pamoja nawe^b na hakuna mtu atakayekushambulia ili kukudhuru; kwa maana nina watu wengi katika jiji hili.” **11** Basi akakaa huko kwa mwaka mmoja na miezi sita, akifundisha neno la Mungu kati yao.

12 Galio alipokuwa liwali* wa Akaya, Wayahudi wakau-ngana, wakamshambulia Paulo na kumpeleka kwenye kiti cha hukumu, **13** wakisema: “Mtu huyu anawashawishi watu wamwabudu Mungu kwa njia iliyo kinyume cha sheria.” **14** Lakini Paulo alipokuwa karibu kuzungumza, Galio akawaambia Wayahudi: “Enyi Wayahudi, kama kweli lingekuwa kosa fulani au uhalifu mkubwa, ningekuwa na sababu ya kuwasikiliza kwa subira. **15** Lakini kama mnabishania maneno na majina na sheria yenu,^c amueni wenyewe. Mimi sitaki kuwa mwamuzi wa mambo hayo.” **16** Ndipo akawafukuza kutoka mbele ya kiti cha hukumu. **17** Basi wote wakamkamata Sosthene,^d ofisa msimamizi wa sinagogi na kuanza kumpiga mbele ya kiti cha hukumu. Lakini Galio hakujihusisha kamwe na mambo hayo.

18:12 *Gavana Mroma aliyetawala mkoa. Angalia Kamusi, uku. 2012.

18 Hata hivyo, baada ya kukaa siku kadhaa, Paulo aliwaaga akina ndugu naye akasafiri baharini kwenda Siria, pamoja na Prisila na Akila. Alikuwa amekata nywele zake huko Kenkrea,^a kwa sababu alikuwa ameweka nadhiri. **19** Basi wakafika Efeso, akawaacha huko; lakini yeye akaingia ndani ya sinagogi na kujadiliana na Wayahudi.^b **20** Ingawa waliendelea kumsihi akae kwa muda mrefu zaidi, hakukubali **21** bali aliwaaga na kuwaambia: "Nitarudi kwenu tena, Yehova* akipe nda." Naye akasafiri baharini kutoka Efeso **22** na kushuka mpaka Kaisaria. Akapanda kwenda na kulisalimia kutaniko,* kisha akashuka kwenda Antiokia.^c

23 Baada ya kukaa huko kwa muda fulani, akaondoka na kwenda sehemu mbalimbali katika nchi ya Galatia na Frigia,^d akiwaimarisha wanafunzi wote.^e

24 Sasa Myahudi aliyetitwa Apolo,^f mzaliwa wa Aleksandria akafika Efeso; alikuwa mwanamume mwenye ufasaha na ujuzi mwingi wa Maandiko. **25** Mwanamume huyu alikuwa amefundishwa^g njia ya Yehova,* na akiwa amewaka roho, alikuwa akizungumza na kufundisha kwa usahihi kumhusu Yesu, lakini alifahamu ubatizo wa Yohana tu. **26** Akaanza kuzungumza kwa ujasiri katika sinagogi, nao Prisila na Akila^g walipomsikia, wakamchukua na kumfanulia kwa usahihi zaidi njia

18:21, 25 *Angalia Nyongeza A5.
18:22 *Inaonekana alienda Yerusalemu.
18:25 ^gAu "amefundishwa kwa mdomo."

SURA YA 18

a Ro 16:1

b Mdo 17:2

c Mdo 15:36

d Mdo 16:6

e Mdo 14:21, 22
Mdo 15:32f Mdo 19:1
1Ko 1:12
1Ko 3:5, 6g Ro 16:3
1Ko 16:19

Safu ya 2

a Kum 18:15
Zb 16:10
Isa 7:14
Mik 5:2

SURA YA 19

b Mdo 18:24
1Ko 3:5, 6

c 1Ko 16:8, 9

d Mdo 2:38

e Mdo 18:24, 25

f Mt 3:11
Mk 1:4

g Yoh 1:15, 30

h Mdo 8:14, 17

i Mdo 2:1, 4
Mdo 10:45, 46
1Ko 12:8, 10

j Mdo 17:2

k Mdo 1:3
Mdo 28:30, 31

ya Mungu. **27** Pia, kwa sababu alitaka kuvuka kwenda Akaya, akina ndugu wakawaandikia wanafunzi wakiwahimiza wamkaribishe kwa fadhili. Basi alipofika huko, akawaaidia sana wale ambao kupitia fadhili zisizostahiliwa za Mungu walikuwa wameamini; **28** kwa maana alithibitisha kikamili hadharani na kwa juhudi nyingi kwamba Wayahudi walikuwa wamekosea, na kuwaonyesha kwa Maandiko kuwa Yesu ndiye Kristo.^a

19 Apolo^b alipokuwa Korintho, Paulo alipita bara na kushuka mpaka Efeso.^c Aliwakuta wanafunzi fulani huko **2** akawauliza: "Mlipoa nza kuamini, je, mlipokea roho takatifu?"^d Wakamjibu: "Hata hatujasikia kwamba kuna roho takatifu." **3** Basi akawauliza: "Mlibatizwa katika nini?" Wakajibu: "Katika ubatizo wa Yohana."^e **4** Paulo akasema: "Yohana aliubatiza watu ili kuonyesha kwamba wametubu,^f akiwaambia wamwamini yule ambaye angekuja baada yake,^g yaani, Yesu." **5** Waliposikia hivyo, wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu. **6** Paulo alipoweka mikono juu yao, wakapokea roho takatifu,^h nao wakaanza kuzungumza kwa lugha za kigeni na kutoa unabii.ⁱ **7** Wote walikuwa wanaueme karibu **12**.

8 Akaingia katika sinagogi,^j na kwa miezi mitatu akazungumza kwa ujasiri, akitoa hotuba na kujadiliana kwa ushawishi kuhusu Ufalme wa Mungu.^k **9** Lakini baadhi yao wakawa wagumu* na wakaka-

19:9 *Au "wakawa wakaidi."

taa kuamini, huku wakizungu-mza vibaya kuhusu Ile Njia^a mbele ya umati. Basi akawaacha^b na kuwatenga wanafunzi kutoka kwao, na kila siku alikuwa akitoa hotuba katika ukumbi wa shule ya Tiranu. **10** Aliendelea kufanya hivyo kwa miaka miwili, hivi kwamba wote walioishi katika mkoa wa Asia wakasikia neno la Bwana, Wayahudi na Wagiriki pia.

11 Na Mungu akaendelea kufanya matendo yenye nguvu yasiyo ya kawaida kupitia mikono ya Paulo,^c **12** hivi kwamba hata nguo na vitambaa vilivyogusa mwili wake vilipelekewa wagonjwa,^d nao wapakonywa magonjwa, na roho waovu wakatoka.^e **13** Lakini baadhi ya Wayahudi waliosafiri huku na huku wakifukuzi roho waovu wakajaribu pia kutumia jina la Bwana Yesu kwa wale waliokuwa na roho waovu; wakisema: "Ninakuumuru kwa jina la Yesu ambaye Paulo humhubiri."^f **14** Wana saba wa Skewa, mkuu wa makuhani wa Kiyahudi, walikuwa wakifanya hivyo. **15** Lakini yule roho mwovu akawaambia: "Ninamjua Yesu^g nami ninamfahamu Paulo;^h lakini ninyi ni nani?" **16** Ndi-po mtu huyo aliyekuwa na roho mwovu akawarukia, akawazidi nguvu mmoja baada ya mwingine na kuwashinda, hivi kwamba wakatoka mbio katika nyumba hiyo wakiwa uchi na wakiwa wameumizwa. **17** Watu wote waka-jua jambo hilo, Wayahudi na Wagiriki walioishi huko Efeso; na wote wakaogopa, nalo jina la Bwana Yesu likaendelea ku-

SURA YA 19

a Mdo 9:1, 2
Mdo 22:4

b Mt 10:14

c Mdo 14:3

d Mk 6:56
Mdo 5:15

e Mt 10:1

f Mdo 16:18

g Mt 8:28, 29
Mk 1:23, 24
Lu 4:33, 34

h Mdo 16:16, 17

Safu ya 2

a Kum 18:10, 11

b Mdo 6:7
Mdo 12:24
Kol 1:6

c 1Ko 16:5

d Mdo 20:22

e Mdo 23:11

f Mdo 16:1, 2

g 2Ti 4:20

h 2Ko 1:8

i Mdo 9:1, 2
Mdo 19:9
Mdo 22:4

j Mdo 16:16

k Efe 1:1

tukuzwa. **18** Na wengi kati ya wale waliokuwa waamini walikuwa wakija na kuungama, wakieleza waziwazi kuhusu mazoea yao. **19** Kwa kweli, idadi kubwa ya wale waliozoea kufanya uchawi wakakusanya vitabu vyao pamoja na kuviteketeza mbele ya kila mtu.^a Nao wakafanya hesabu na kupata vitabu hivyo vilikuwa na thamani ya vipande 50,000 vya fedha. **20** Hivyo kwa njia yenye nguvu, neno la Yehova* likazidi kukua na kusitawi.^b

21 Baada ya mambo hayo kutukia, Paulo akaazimia katika roho yake kwamba baada ya kupitia Makedonia^c na Akaya, atasafiri kwenda Yerusalemu.^d Akasema: "Baada ya kwenda huko, lazima pia nione Roma."^e **22** Basi akawatumawili kati ya wale walio-mhudumia, Timotheo^f na Erasto,^g waende Makedonia lakini yeye akakaa kwa muda fulani katika mkoa wa Asia.

23 Wakati huo kukatokea mvurugo^h mkubwa kuhusu Ile Njia.ⁱ **24** Kwa maana mtu fulani aliyelitwa Demetrio, fundi wa fedha aliyetengeneza vihekalu vya fedha vya Artemi, aliwaletea mafundi faida kubwa.^j **25** Akawakusanya pamoja na wengine waliofanya kazi kama hiyo na kuwaambia: "Wanaume, mnajua vema kwamba tunapata mafanikio yetu kutokana na biashara hii. **26** Sasa mnaona na kusikia kwamba si katika Efeso tu,^k bali pia katika karibu mkoa wote wa Asia, Paulo huyu ameushawishi umati mkubwa na kuwafanya wawe na maoni

19:20 * Angalia Nyongeza A5.

tofauti, akisema kwamba miungu iliyotengenezwa kwa mkono, kwa kweli si miungu.^a

27 Isitoshe, kuna hatari kwamba biashara yetu itapata sifa mbaya na pia hekalu la Artemi mungu mkuu wa kike litao-nwa kuwa si kitu, naye ana-yeabudiwa katika mkoa wote wa Asia na dunia inayokaliwa atakosa utukufu.” **28** Waliposikia jambo hilo wakajawa na hasira, nao wakaanza kusema kwa sauti kubwa: “Artemi wa Waefeso ni mkuu!”

29 Basi jiji likajaa mvurugo na wote pamoja wakakimbia na kuingia katika ukumbi wa maonyesho, wakiwakokota Gayo na Aristarko,^b Wamakedonia waliokuwa wakisafiri pamoja na Paulo.

30 Naye Paulo alitaka kuingia walimokuwa watu hao, lakini wanafunzi hawakumruhusu.

31 Hata baadhi ya wasimamizi wa sherehe na michezo waliomtendea kwa urafiki, wakamtumia ujumbe wakimsihi asijihatarishe kwa kuingia katika ukumbi wa maonyesho.

32 Kwa kweli, baadhi yao walikuwa wakisema kwa sauti kubwa jambo moja na wengine jambo tofauti; kwa maana kusanyiko hilo lilikuwa limevurugika, na wengi wao hawakujua kwa nini walikuwa wamekusanyika.

33 Basi wakamtoa Aleksanda kwenye umati, huku Wayahudi wakimsukuma mbele, naye Aleksanda akapunga mkono akitaka kujitetea mbele ya watu.

34 Lakini walipotambua kwamba alikuwa Myahudi, wote wakaanza kupaza sauti kwa pamoja kwa karibu saa mbili wakisema: “Artemi wa Waefeso ni mkuu!”

SURA YA 19

a Mdo 17:29
1Ko 8:4

35 Mwishowe, karani wa jiji akaunyamazisha umati, kisha akasema: “Watu wa Efeso, kwa kweli ni nani kati ya wanadamu ambaye hajui kwamba jiji la Efeso ndilo mlinsi wa hekalu la Artemi mkuu na sanamu iliyoanguka kutoka mbinguni?” **36** Kwa kuwa mambo haya hayawezi kukanushwa, tulieni na msitende haraka haraka. **37** Kwa maana mmewaleta hapa watu hawa ambao hawaibi katika mahekalu wala kumkufuru mungu wetu wa kike.

38 Basi ikiwa Demetrio^a na mafundi walio pamoja naye wana kesi dhidi ya mtu fulani, siku za mahakama hufanywa na kuna maliwali;* wanaweza kushtakiana huko. **39** Lakini ikiwa mnatafuta jambo lingine zaidi ya hilo, linapaswa kuamuliwa katika kusanyiko la kawaida. **40** Kwa kweli tunakabili hatari ya kushtakiwa kwa uchochezi kuhusu tukio la leo, kwa sababu hatuna msingi wa kuwa na kikundi hiki chenye machafuko.”

41 Baada ya kusema mambo hayo, akauagiza umati utawanyike.

20 Baada ya ghasia kutulia, Paulo akatuma watu wawaite wanafunzi, akawatia moyo na kuwaaga, kisha akanza safari yake ya kwenda Makedonia. **2** Baada ya kupitia maeneo hayo na kuwatia moyo kwa maneno mengi wale waliokuwa huko, akafika Ugiriki. **3** Akakaa huko miezi mitatu, lakini kwa sababu Wayahudi walikuwa wametunga hila dhidi yake^b ali-

b Mdo 20:4
Kol 4:10
Flm 23, 24

Safu ya 2

a Mdo 19:24

SURA YA 20

b Mdo 23:12, 16
2Ko 11:23, 26

19:38 *Liwali alikuwa gavana Mroma aliyetawala mkoa. Angalia Kamusi, uku. 2012.

pokuwa karibu kusafiri kwen-
nda Siria, akaamua kurudi ku-
pitia Makedonia. **4** Alienda
pamoja na Sopatro mwana wa
Piro wa Beroya, Aristarko^a
na Sekundo wa Wathesaloni-
ke, Gayo wa Derbe, Timotheo^b
na, kutoka wilaya ya Asia, Ti-
kiko^c na Trofimo.^d **5** Wanau-
me hao wakatangulia na ku-
tushiriki huko Troa; **6** lakini
sisi tukaanza kusafiri bahari-
ni kutoka Filipi baada ya She-
rehe ya Mikate Isiyo na Sha-
chu,^e siku tano baadaye tu-
kawafikia huko Troa, tukakaa
huko siku saba.

7 Siku ya kwanza ya juma,
tulipokuwa tumekusanyika ili
kupata mlo, Paulo akaan-
za kuwahutubia, kwa sababu
angeondoka kesho yake; naye
akarefusha hotuba yake mpa-
ka katikati ya usiku. **8** Basi
kulikuwa na taa nyingi katika
chumba cha juu tulimokuwa
tumekusanyika. **9** Kijana ai-
twaye Eutiko alikuwa ameketi
dirishani, naye akalala usingi-
zi mzito Paulo alipokuwa
akiongea, basi akalemewa na
usingizi, akaanguka chini ku-
toka ghorofa ya tatu, akaoko-
twa akiwa amekufa. **10** La-
kini Paulo akashuka kutoka
ghorofani, akajitupa juu yake
akamkumbatia^f na kusema:
“Acheni kupiga kelele, kwa
maana yuko hai.”^g **11** Ki-
sha akapanda ghorofani,
akaanzisha mlo* na kula cha-
kula. Akaendelea kuzungu-
mza kwa muda mrefu, mpa-
ka mapambazuko, kisha akaon-
doka. **12** Basi wakamchu-
kua mvulana huyo akiwa hai,
wakafarijika sana.

20:10 *Au “nafsi yake imo ndani yake.”
20:11 *Tnn., “akaumea mkate.”

SURA YA 20

a Mdo 27:2

b Mdo 16:1, 2

c Efe 6:21
Kol 4:7
2Ti 4:12d Mdo 21:29
2Ti 4:20e Kut 12:15
Kut 23:15f 1Fa 17:21, 22
2Fa 4:32, 34g Mt 9:23, 24
Yoh 11:39, 40
Mdo 9:39, 40

Safu ya 2

a Mdo 18:21

b Mdo 24:17

c Mdo 19:9, 10

d 1Ko 15:9
1Th 2:6e Mt 28:19, 20
2Ti 4:2

f Mdo 5:42

g Mk 1:14, 15

h Lu 24:46, 47

13 Sasa tukaenda kwenye
meli na kusafiri mpaka Aso,
ambako tulikusudia kumchu-
kua Paulo, kwa maana baada
ya kutuagiza hivyo, alikusu-
dia kwenda huko kwa miguu.
14 Basi alipotufikia huko
Aso, akapanda kwenye meli
tulimokuwa, tukaenda Mitile-
ne. **15** Tukaondoka huko ke-
sho yake, tukafika karibu na
Kio, lakini siku ya pili tuka-
fika Samo, na siku iliyofua-
ta tukafika Mileto. **16** Paulo
alikuwa ameamua kuendelea
na safari bila kupitia Efeso,^a
ili asitumie muda wowote ka-
tika mkoa wa Asia, kwa ma-
ana alikuwa akiharakisha kufi-
ka Yerusalemu^b siku ya Shere-
he ya Pentekoste kama inge-
wezekana.

17 Hata hivyo, kutoka Mile-
to akatuma watu kwenda Efe-
so wawaite wazee wa kutani-
ko hilo waje. **18** Walipokuja
akawaambia: “Mnajua vema ji-
nsi nilivyotenda kati yenu tan-
gu siku ya kwanza niliyokan-
yaga mkoa wa Asia,^c **19** ni-
livyomtumikia Bwana kwa
unyenyekevu wote^d na ma-
chozi na majaribu yaliyonip-
ata kupitia hila za Waya-
hudi, **20** nami sikuepuka ku-
waambia ninyi jambo lolote
lenye faida* na kuwafun-
disha hadharani^e na nyumba
kwa nyumba.^f **21** Lakini nili-
toa ushahidi kikamili kwa
Wayahudi na Wagiriki kuhu-
su toba^g kwa Mungu na
kuwa na imani katika Bwa-
na wetu Yesu.^h **22** Na sasa,
tazameni! nikiwa nimefu-
ngwa katika* roho, ninasafiri

20:19 *Au “unyenyekevu wa akili.”
20:20 *Au “kwa faida yenu.” 20:22
*Au “nimechochewa na.”

kwenda Yerusalemu, ingawa sijui mambo yatakayonipata huko, **23** isipokuwa kutoka jiji mpaka jiji roho takatifu inanitolea ushahidi tena na tena, ikisema kwamba nitafungwa gerezeni na kupatwa na dhiki.^a **24** Hata hivyo, sioni uhai wangu* kuwa muhimu kwangu,[#] mradi tu nimalize mwendo wangu^b na huduma niliyopokea kutoka kwa Bwana Yesu, kutoa ushahidi kamili kuhusu habari njema ya fadhili zisizostahiliwa za Mungu.

25 "Na sasa, tazameni! ninajua kwamba hakuna yeyote kati yenu ninyi niliowahubiria kuhusu Ufalme atakayeona uso wangu tena. **26** Basi ninawaita ili mshuhudie leo hii kwamba mimi sina hatia ya damu ya mtu yeyote.^c **27** kwa maana sikukosa kuwaambia mashauri yote ya* Mungu.^d **28** Jialieni wenyewe^e na kundi lote, ambalo kati yake roho takatifu imewaweka ninyi rasmi muwe waangalizi,^f mlichunge kutaniko la Mungu,^g ambalo alilunua kwa damu ya Mwana wake mwenyewe.^h **29** Ninajua kwamba nitakapoondoka mbwamwitu wenye kukandamiza wataingia miongoni mwenuⁱ nao hawatalitendea kundi kwa wororo, **30** na kutoka miongoni mwenu watu watasimama na kusema mambo yaliyopotoka ili kuwavuta wanafunzi wawafuate wao wenyewe.^j

31 "Kwa hiyo endeleeni kukesha, na kukumbuka kwa-

20:24 *Au "nafsi yangu." #Au "ukiwa na thamani yoyote kwangu." **20:27** *Au "kusudi lote la."

SURA YA 20

a Mdo 9:15, 16
Mdo 21:4, 11

b 2Ti 4:7

c Eze 33:8

d Mt 28:19, 20

e 1Ti 4:16

f 1Ti 3:1-7
Tit 1:5-9
Ebr 13:17

g Yoh 21:15
Efe 4:11
1Pe 5:2-4

h Mt 26:27, 28
1Yo 1:7

i Mt 7:15
2Th 2:3
2Pe 2:1

j 1Ti 4:1
2Ti 4:3, 4
1Yo 2:18, 19

Safu ya 2

a Mdo 19:9, 10

b Efe 1:18
Kol 1:12

c 1Sa 12:1, 3
Mt 10:8
1Ko 9:11, 12
2Ko 7:2
Tit 1:7

d Mdo 18:3
1Ko 4:11, 12
1Th 2:9

e Efe 4:28
1Th 4:11, 12
2Th 3:7, 8

f Met 19:17
Mt 10:8
Lu 6:38

g Mdo 20:25

mba kwa miaka mitatu,^a usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mmoja wenu kwa machozi. **32** Na sasa ninawakabidhi ninyi kwa Mungu na kwa neno la fadhili zake zisizostahiliwa, ambalo linaweza kuwajenga na kuwapa urithi kati ya wale wote walio-takaswa.^b **33** Sikutamani fedha, dhahabu, wala mavazi ya mtu yeyote.^c **34** Ninyi wenyewe mnajua kwamba nimefanya kazi kwa hii mikono yangu ili kupata mahitaji yangu^d na ya wale walio pamoja nami. **35** Nimewaonyesha ninyi katika mambo yote kwamba kwa kufanya kazi kwa bidii hivyo,^e ni lazima mwasaidie walio dhaifu, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, aliposema: "Kuna furaha zaidi katika kutoa^f kuliko ilivyo katika kupokea."

36 Baada ya kusema mambo haya, akapiga magoti pamoja nao wote na kusali. **37** Kwa kweli, wote wakalia sana, nao wakamkumbatia Paulo* na kumbusu kwa upendo,[#] **38** kwa maana waliumia sana aliposema kwamba hawangeuona uso wake tena.^g Kisha wakamsindikiza mpaka kwenye meli.

21 Tulipofaulu kuachana nao na kusafiri baharini, tulienda moja kwa moja mpaka Kosi, siku iliyofuata tukafika Rode, na kutoka huko tukaenda Patara. **2** Tulipopata meli iliyokuwa ikivuka kwenda Foinike, tukapanda na kuondoka. **3** Baada ya kufika mahali tulipoweza kuona kisiwa cha Kipro, tukakia-

20:37 *Tnn., "wakamwangukia Paulo shingoni." #Au "wororo."

cha upande wa kushoto tukasafiri mpaka Siria, tukafika Tiro ambako meli ilipaswa kushusha shehena. **4** Tukawatafuta wanafunzi na tulipowapata tukakaa huko siku saba. Lakini kupitia roho, wakamwambia Paulo tena na tena asikanyage Yerusalemu.^a **5** Baada ya muda wetu huko kwisha, tukaondoka na kuanza safari, lakini wote kutia ndani wana wake na watoto, wakatusindikiza mpaka nje ya jiji. Tukapiga magoti ufuoni, tukasali, **6** kisha tukaagana. Tukapanda meli, nao wakarudi nyumbani kwao.

7 Ndipo tukakamilisha safari ya baharini kutoka Tiro tukafika Tolemai, tukawasalimu akina ndugu na kukaa nao siku moja. **8** Siku iliyofuata tukaondoka na kufika Kaisaria, tukaingia katika nyumba ya Filipo mweneza-injili, aliye kuwa mmoja wa wale wanau-me saba,^b nasi tukakaa pamoja naye. **9** Mtu huyo alikuwa na binti wanne ambao hawakuwa wamelewa,* nao walitoa unabii.^c **10** Lakini baada ya kukaa huko kwa siku kadhaa, nabii aliyeitwa Agabo^d akashuka kutoka Yudea. **11** Akaja mahali tulipokuwa akachukua mshipi wa Paulo, akajifunga miguu na mikononi na kusema: "Hivi ndivyo roho takatifu inavyosema, 'Wayahudi kule Yerusalemu watamfunga^e hivi mwanamume ambaye mshipi huu ni wake, nao watamtia mikononi mwa watu wa mataifa.'"^f **12** Tuliposikia hayo, sisi na wale waliokuwa hapo tukaanza kumsihi Paulo asipande kwenda

21:9 *Tnn., "walikuwa mabikira."

SURA YA 21

a Mdo 21:10-12

b Mdo 6:3, 5

c Yoe 2:28
Mdo 2:17
1Ko 11:5

d Mdo 11:27, 28

e Mdo 20:22, 23
Mdo 21:33

f Mdo 9:15, 16

Safu ya 2

a Mdo 20:24
2Ko 4:10, 11
2Ti 4:6

b Mdo 12:17
Mdo 15:13
Gal 1:19
Gal 2:9
Yak 1:1

c Mdo 15:1

d Ro 2:28, 29
1Ko 7:18-20

Yerusalemu. **13** Kisha Paulo akasema: "Kwa nini mnalia na kujaribu kunivunja moyo?*" Muwe na hakika kwamba niko tayari si kufungwa tu bali pia kufa huko Yerusalemu kwa ajili ya jina la Bwana Yesu."^a **14** Tuliposhindwa kumshawishi, tukaacha kumkataza,* tukasema: "Mapenzi ya Yehova[#] na yatendeke."

15 Sasa baada ya siku hizo tukajitayarisha kwa ajili ya safari kisha tukaanza kuelekea Yerusalemu. **16** Baadhi ya wanafunzi kutoka Kaisaria wakaenda pamoja nasi, waka-tupeleka kwa Mnasoni wa Kipro, mwanafunzi wa zamani ambaye tulipaswa kuwa wageni nyumbani kwake. **17** Tulipofika Yerusalemu, akina ndugu wakatukaribisha kwa furaha. **18** Lakini siku iliyo fuata Paulo akaingia pamoja nasi kwa Yakobo,^b na wazee wote walikuwapo. **19** Akawasalimu na kuanza kusimulia kirefu mambo ambayo Mungu alifanya miongoni mwa mataifa kupitia huduma yake.

20 Baada ya kusikia jambo hilo, wakaanza kumtukuzia Mungu, lakini wakamwambia: "Ndugu, unaona jinsi ambavyo maelfu ya Wayahudi wamekuwa waamini, na wote wanafuata Sheria kwa bidii.^c **21** Lakini wamesikia uvumi kukuhusu kwamba umekuwa ukiwafundisha Wayahudi wote kati ya mataifa kuiasi sheria ya Musa, ukiwaambia wasiwatahiri watoto wao wala kufuata desturi zilizowekwa.^d **22** Sasa tufanye nini? Kwa kweli watasikia

21:13 *Au "kuudhoofisha moyo wangu."

21:14 *Tnn., "tukakaa kimya." [#]Angalia Nyongeza A5.

kwamba umefika. **23** Basi fanya jambo tunalokuambia: Tuna wanaume wanne waliojiwekea nadhiri. **24** Nenda pamoja na watu hawa ukajitakase kisherehe pamoja nao na kuwagharimia, ili wanyolewe vichwa vyao. Ndipo kila mtu atajua kwamba uvumi walioambiwa kukuhusu si wa kweli, bali unatembea kwa utaratibu, na pia unashika Sheria.^a **25** Kuhusu waamini kutoka kati ya mataifa, tumewatumia uamuzi wetu kwa maandishi kwamba wanapaswa kuepuka vitu vilivyotolewa dhabihu kwa sanamu^b na pia damu,^c na vitu vilivyonyongwa,^d na uasherati.”^e

26 Ndipo Paulo akaenda pamoja na wanaume hao siku iliyofuata, akajitakasa kisherehe pamoja nao,^f naye akaingia hekaluni ili kutoa taarifa kuhusu wakati ambapo siku za kujitakasa zingekwisha na toleo litolewe kwa ajili ya kila mmoja wao.

27 Sasa zile siku saba zilipokaribia kwisha, Wayahudi kutoka Asia walipomwona hekaluni, wakauchoea umati wote, nao wakamkamata, **28** wakisema kwa sauti kubwa: “Wanaume wa Israeli, tusaidieni! Huyu ndiye mwanaume anayewafundisha watu kila mahali dhidi ya watu wetu na Sheria yetu na mahali hapa. Isitoshe, hata aliwaingiza Wagiriki hekaluni naye amepatia unajisi mahali hapa patakatifu.”^g **29** Kwa maana mwanzoni walikuwa wamemwona Trofimo^h Mwefeso jiji-

21:25 *Au “ vitu vilivyokuwa bila kutolewa damu.” ^aNeno la Kigiriki *pornei*’a. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 21

a 1Ko 9:20

b Mwa 35:2
Kut 34:15c Mwa 9:4
Law 3:17
Law 17:10
1Sa 14:32, 33d Law 17:13
Kum 12:23, 24e Mdo 15:28, 29
1Ko 6:9
Kol 3:5
1Th 4:3
1Pe 4:3

f 1Ko 9:20

g Mdo 24:5, 6

h Mdo 20:4
2Ti 4:20

Safu ya 2

a Mdo 20:22, 23
Mdo 21:10, 11

ni akiwa pamoja naye, nao wakadhani Paulo alikuwa amewingiza hekaluni. **30** Jiji lote likawa na machafuko, watu wakakimbia pamoja wakamkamata Paulo na kumkota nje ya hekalu, na mara moja milango ikafungwa. **31** Walipokuwa wakijaribu kumuua, kamanda wa kikosi cha jeshi akapata habari kwamba Yerusalemu yote ilikuwa na vurugu; **32** mara moja akachukua wanajeshi na mafisa wa jeshi wakakimbia kwenenda huko. Walipomwona kamanda wa jeshi na wanajeshi, wakaacha kumpiga Paulo.

33 Ndipo yule kamanda wa jeshi akakaribia akamweka chini ya ulinzi na kuamuru afungwe kwa minyororo miwili;^a kisha akauliza huyo ni nani na alikuwa amefanya nini. **34** Lakini baadhi ya watu katika umati wakaanza kusema jambo moja kwa sauti kubwa na wengine jambo tofauti. Basi aliposhindwa kujua jambo lolote la hakika kwa sababu ya fujo hizo, akaamuru aletwe kwenye makao ya wanajeshi. **35** Lakini alipofika kwenye ngazi, alilazimika kubebwa na wanajeshi kwa sababu umati ulitaka kumuuzima, **36** kwa maana umati wa watu uliendelea kuwafuata, ukisema kwa sauti kubwa: “Auawe!”

37 Alipokuwa karibu kuingizwa katika makao ya wanajeshi, Paulo akamuuliza yule kamanda wa jeshi: “Je, ninaruhusiwa kukuambia jambo fulani?” Naye akamuuliza: “Je, unajua kuzungumza Kigiriki? **38** Kwani wewe si yule Mmisi ambaye hivi majuzi alianzi-

sha uchochezi na kuwaongoza wale wanaume 4,000 wenye visu hadi nyikani?" **39** Paulo akamjibu: "Mimi kwa kweli ni Myahudi,^a wa Tarso^b huko Kilikia, raia wa jiji maarufu. Basi nakuomba uniruhusu nizingumze na watu hawa." **40** Baada ya kupewa ruhusa, Paulo, akiwa amesimama kwenye ngazi, akawapungia watu mkono. Waliponyamaza kabisa, akawahutubia kwa lugha ya Kiebrania,^c akisema:

22 "Wanaume, akina ndugu na akina baba, nisi-kilizeni ninapojitetea mbele yenu sasa."^d **2** Basi, waliposikia anazungumza nao kwa lugha ya Kiebrania, wakazidi kukaa kimya, naye akasema: **3** "Mimi ni Myahudi,^e aliyezaliwa huko Tarso ya Kilikia,^f nilielimishwa katika jiji hili miguuni pa Gamalieli,^g na kufundishwa kwa usahihi kabisa Sheria ya mababu,^h nikiwa na bidii kwa ajili ya Mungu kama nyote mlivyo leo.ⁱ **4** Niliitese Njia hii kufikia kifo, nikiwafunga na kuwatia magerezani wanaume na wanawake pia,^j **5** kama vile kuhani mkuu na kusanyiko lote la wazee wanavyoweza kutoa ushahidi. Nili-pata pia barua kutoka kwao ili nizipeleke kwa akina ndugu huko Damasko, nami nilikuwa ninaenda kuwakamata wale waliokuwa huko na kuwaleta Yerusalemu wakiwa wamefungwa ili waadhibiwe.

6 "Lakini nilipokuwa safarini nikikaribia kufika Damasko, karibu katikati ya mchana, ghafla nuru kubwa kutoka mbinguni ikamulika kunzunguka,^k **7** nami nikaanguka chini na kusikia sauti ikiniuli-

SURA YA 21

a Flp 3:4, 5

b Mdo 22:3

c Mdo 26:14

SURA YA 22

d Flp 1:7

e Ro 11:1

f Mdo 21:39

g Mdo 5:34

h Mdo 26:4, 5

i Gal 1:14
Flp 3:4-6j Mdo 8:3
Mdo 9:1, 2
Mdo 26:9-11
1Ti 1:12, 13k Mdo 9:3-8
Mdo 26:13-15

Safu ya 2

a Mdo 26:16

b Mdo 9:17, 18

c 1Ko 9:1
1Ko 15:8
Gal 1:15, 16d Mdo 23:11
Mdo 26:16e 1Ko 6:11
1Yo 1:7
Ufu 1:5

f Mdo 10:43

g Mdo 9:26
Gal 1:18

za: 'Sauli, Sauli, kwa nini unanitesa?' **8** Nikajibu: 'Wewe ni nani Bwana?' Naye akania-mbia: 'Mimi ni Yesu Mnazareti, ambaye unamtesa.' **9** Basi watu waliokuwa pamoja nami, waliiona ile nuru lakini hawakuisikia sauti ya yule aliyezungumza nami. **10** Ndipo nikamuuliza: 'Nifanye nini Bwana?' Bwana akania-mbia: 'Simama, uende Damasko, na huko utaambiwa kila kitu ambacho umepangiwa kufanya.'^a **11** Lakini kwa kuwa sikuweza kuona chochote kwa sababu ya utukufu wa nuru hiyo, wale waliokuwa pamoja nami wakanishika mkono na kuniongoza mpaka Damasko.

12 "Kisha mwanamume anayelitwa Anania, aliyemwogopa Mungu kulingana na Sheria, na kushuhudiwa vema na Wayahudi wote walioishi huko, **13** akaja nilipokuwa. Akasi-mama kando yangu, akania-mbia, 'Sauli ndugu, anza kuona tena!' Papo hapo nikatazama juu nikamwona.^b **14** Akasema: 'Mungu wa mababu zetu amekuchagua ujue mape-nzi yake na umwone yule aliyemwadilifu^c na kuisikia sauti ya kinywa chake, **15** kwa sababu utakuwa shahidi wake kwa watu wote kuhusu mambo ambayo umeona na kusikia.^d **16** Na sasa kwa nini unakawia? Simama, ubatizwe na uoshe dhambi zako^e kwa kuliitia jina lake.'^f

17 "Lakini niliporudi Yerusalemu,^g nikiwa ninasali hekaluni, nikapata njozi **18** na kumwona Bwana akiniambia: 'Fanya upesi uondoke Yerusalemu haraka, kwa sababu

hawatakubali ushahidi wako kunihusu.^a **19** Nami nikasema: ‘Bwana, wao wenyewe wanajua vema kwamba nilikuwa nikiwatia gerezani na kuwapiga viboko katika sinagogi moja baada ya lingine wale waliokuamini.’^b **20** na damu ya Stefano shahidi wako ilipokuwa ikimwagwa, nilikuwa nimesimama kando na kukubaliana na jambo hilo nikiyalinda mavazi ya nje ya wale waliokuwa wakimuuu.^c **21** Na bado akaniambia: ‘Nenda kwa sababu nitakutuma kwa maifa yaliyo mbali.’^d

22 Basi wakaendelea kumsikiliza mpaka aliposema maneno hayo. Kisha wakasema kwa sauti kubwa: “Mwondoeni duniani mtu kama huyu, hafai kuishi!” **23** Kwa sababu walikuwa wakipiga kelele na kutupa mavazi yao ya nje huku na huku na kurusha mavumbi hewani,^e **24** yule kamanda wa jeshi akaagiza Paulo aingizwe katika makao ya wanajeshi na kuamuru ahajiwe huku akipigwa mijeledi, ili ajue kwa nini hasa walikuwa wakimpigia Paulo kelele hivyo. **25** Lakini walipokuwa wamemnyoosha ili kumpiga mijeledi, Paulo akamuuliza ofisa wa jeshi aliyekuwa amesimama kupo: “Je, ni halali kwenu kumpiga mijeledi Mroma* ambaye hajahukumiwa?”^f **26** Yule ofisa wa jeshi aliposikia hivyo, akaenda kwa kamanda wa jeshi na kuwambia: “Unakusudia kufanya nini? Kwa maana mtu huyu ni Mroma.” **27** Basi kamanda wa jeshi akakaribia na

22:25 *Au “raia Mroma.” ^f Au “bila umuzi wa mahakama.”

SURA YA 22

a Mdo 9:28, 29

b Mdo 8:3

c Mdo 7:58
Mdo 8:1
ITI 1:13, 15d Mdo 9:15
Mdo 13:2
Ro 1:5
Ro 11:13
Gal 2:7
ITI 2:7

e 2Sa 16:13

f Mdo 16:37, 38
Mdo 23:27

Safu ya 2

a Mdo 16:37

b Mdo 25:16

c Mt 10:17, 18
Lu 21:12

SURA YA 23

d Mdo 24:15, 16
Zko 1:12
Ebr 13:18
1Pe 3:16

e Kut 22:28

kumuuliza: “Niambie, wewe ni Mroma?” Akajibu: “Ndiyo.” **28** Kamanda wa jeshi akasema: “Mimi nilinunua haki hizo za kuwa raia kwa pesa nyingi.” Paulo akasema: “Lakini mimi nina haki hizo kwa kuza-liwa.”^a

29 Kwa hiyo, mara moja watu waliokuwa karibu kumhoji kwa kumtesa wakamwacha; na kamanda wa jeshi akaogopa alipotambua kwamba Paulo ni Mroma na kwamba alikuwa amemfunga kwa minyororo.^b

30 Basi siku iliyofuata, kwa kuwa alitaka kujua hasa sababu iliyowafanya Wayahudi wamshtaki, akamfungua na kuwaamuru wakuu wa makuhani na Sanhedrini yote wakusanyike. Kisha akamleta Paulo chini na kumsimamisha kati yao.^c

23 Paulo akaikazia macho Sanhedrini, akasema: “Wanaume, akina ndugu, nitemenda kwa dhamiri safi kabisa^d mbele za Mungu mpaka leo hii.” **2** Ndipo kuhani mkuu Anania akawaagiza wale waliosimama kando yake wampige kofi mdomoni. **3** Paulo akamwambia: “Mungu atakupiga wewe, ewe ukuta uliopakwa chokaa. Je, unaketi kunihukumu kulingana na Sheria na wakati uleule unai-vunja Sheria hiyo kwa kuamuru nipigwe?” **4** Wale waliosimama kando wakamuuliza: “Je, unamtukana kuhani mkuu wa Mungu?” **5** Paulo akasema: “Akina ndugu, siku-jua yeye ni kuhani mkuu. Kwa maana imeandikwa, ‘Usiseme vibaya kuhusu mtawala wa watu wako.’”^e

6 Sasa Paulo, akijua kwamba sehemu moja ilikuwa Masadukayo na nyingine Mafarisayo, akasema kwa sauti kubwa katika Sanhedrini: “Wanaume, akina ndugu, mimi ni Farisayo,^a mwana wa Mafarisayo. Ninahukumiwa kwa sababu ya tumaini la ufufuo wa wafu.” **7** Baada ya kusema hivyo, kukatokea mtengano kati ya Mafarisayo na Masadukayo, na kusanyiko likagawanika. **8** Kwa maana Masadukayo husema hakuna ufufuo wala malaika wala roho, lakini Mafarisayo huyakubali* hayo yote.^b **9** Basi kuka-wa na vurugu, na baadhi ya waandishi wa chama cha Mafarisayo wakasimama na kuanza kubishana kwa ukali, wakisema: “Hatuoni kosa lolote katika mtu huyu, lakini ikiwa roho au malaika alizungumza naye^c—.” **10** Basi mzozo ulipozidi kuongezeka, kamanda wa jeshi akaogopa kwamba watamrarua-rarua Paulo, akaamuru wanajeshi washuke wamnyakue kutoka kati yao kisha wamlete kwenye makao ya wanajeshi.

11 Lakini usiku uliofuata Bwana akasimama kando yake na kumwambia: “Jipe moyo!^d Kwa maana kama vile ambavyo umekuwa ukitoa ushahidi kamili kunihusu katika Yerusalemu, ndivyo utakavyotoa ushahidi huko Roma pia.”^e

12 Ilipofika mchana, Wayahudi wakafanya hila na kujifunga kwa kiapo cha laana, wakisema hawatakula wala kunywa mpaka watakapomuua Paulo. **13** Kulikuwa na watu

SURA YA 23

a Mdo 26:4, 5
Flp 3:4, 5

b Mdo 4:1, 2

c Mdo 22:6, 7
Mdo 22:17, 18

d Mdo 18:9

e Mdo 27:23, 24
Mdo 28:23
Mdo 28:30, 31

Safu ya 2

a Mdo 23:15

zaidi ya 40 waliofanya hila hiyo iliyofungwa kwa kiapo.

14 Watu hao wakaenda kwa wakuu wa makuhani na wazee na kusema: “Tumejifunga kabisa kwa laana* kwamba hatutakula chochote mpaka tutakapomuua Paulo. **15** Basi ninyi pamoja na Sanhedrini mwambieni kamanda wa jeshi amshushe kwenu kana kwamba mnataka kuchunguza zaidi kesi yake. Lakini kabla hajafika, tutakuwa tayari kumuua.”

16 Hata hivyo, mwana wa dada ya Paulo akasikia kuhusu mpango wao wa kumvizia, akaingia kwenye makao ya wanajeshi na kumjulisha Paulo. **17** Kisha Paulo akamwita mmoja wa maofisa wa jeshi na kumwambia: “Mpeleke kijana huyu kwa kamanda wa jeshi, kwa maana ana jambo la kumweleza.” **18** Basi akampeleka kwa kamanda wa jeshi na kusema: “Mfungwa Paulo aliniita na kuniomba nimlete kijana huyu kwako, kwa sababu ana jambo la kuambiana.” **19** Kamanda wa jeshi akamshika mkono akampeleka faraghani na kumuuliza: “Unataka kuniambia nini?” **20** Akasema: “Wayahudi wamekubaliana kukuomba umshushe Paulo kwenye Sanhedrini kesho, kana kwamba wanataka kupata habari zaidi kuhusu kesi yake.^a **21** Lakini usikubali wakushawishi, kwa maana kuna wanaume zaidi ya 40 kati yao walio tayari kumvizia, nao wamejifunga kwa laana* kwamba hawatakula wala kunywa mpaka watakapomuua;^b

23:8 *Au “huyatangaza hadharani.”

b Mdo 23:12

23:14, 21 *Au “kiapo.”

na sasa wako tayari, wakisubiri ruhusa kutoka kwako.”
22 Basi yule kamanda wa jeshi akamwacha kijana huyo aende baada ya kumwagiza: “Usimwambie mtu yeyote kwamba umenijulisha jambo hili.”

23 Akawaita maofisa wawili wa jeshi na kuwaambia: “Wekeni tayari wanajeshi 200 waende moja kwa moja mpaka Kaisaria, pia wapanda farasi 70 na watu 200 wenye mikuki, saa tatu usiku. **24** Pia, andaeni farasi kwa ajili ya Paulo ili asafiri salama mpaka kwa gavana Feliksi.”
25 Naye akaandika barua yenye ujumbe huu:

26 “Klaudio Lisia kwa Mtukufu, Gavana Feliksi: Salamu! **27** Mwanamume huyu alikamatwa na Wayahudi nao walikuwa karibu kumuua, lakini nikaja haraka pamoja na wanajeshi wangu na kumwoko, ^a baada ya kujua kwamba ni Mroma. **28** Nilitaka kujua kwa nini walikuwa wakimshtaki, basi nikampeleka kwenye Sanhedrini yao. **29** Nikatambua kwamba ameshtakiwa kuhusu maswali ya Sheria yao, ^d lakini hajashtakiwa kwa jambo lolote linalostahili kifo au kufungwa gerezani. **30** Lakini kwa sababu nimejulishwa njama iliyo-pangwa dhidi ya mwanamume huyu, ^e ninamtuma kwako mara moja, na kuwaamuru wale wanaomshtaki wamshtaki mbele yako.”

31 Basi wale wanajeshi wakamchukua Paulo ^f usiku kama walivyoagizwa wakamleta mpaka Antipatri. **32** Siku iliyofuata wakawa-

SURA YA 23

a Mdo 21:31-33

b Mdo 16:37
Mdo 22:25

c Mdo 22:30

d Mdo 25:19

e Mdo 23:16

f Mdo 23:23, 24

Safu ya 2

a Mdo 21:39
Mdo 22:3

b Mdo 24:1

SURA YA 24

c Mdo 23:2

d Mdo 23:26

e Mt 5:11
Mdo 16:20, 21
Mdo 17:6, 7

f Lu 23:1, 2

g Mt 2:23
Mdo 28:22

h Mdo 21:27, 28

ruhusu wapanda farasi wae-
 nde pamoja naye, nao wakaru-
 di kwenye makao ya wanajeshi. **33** Wale wapanda farasi wakaingia Kaisaria, wakamkabidhi gavana ile barua na kumleta Paulo mbele yake. **34** Basi akaisoma na kuuliza ametoka mkoa gani, akajua kwamba alikuwa ametoka Kilikia. ^a **35** Akasema: “Nitasikiliza kesi yako kwa makini wale wanaokushtaki watakopofika.” ^b Naye akaamuru awekwe chini ya ulinzi katika jumba la kifalme la Herode.

24 Siku tano baadaye kuhani mkuu Anania ^c akashuka pamoja na baadhi ya wazee na msemaji wa hadharani* aliyeitwa Tertulo, nao wakawasilisha kesi yao dhidi ya Paulo mbele ya gavana. ^d

2 Alipoitwa, Tertulo akaanza kumshtaki, akisema:

“Kwa kuwa tunafurahia amani nyingi kupitia kwako, na kwa busara yako mabadiliko yanatokea katika taifa hili, **3** nyakati zote na kila mahali tunatambua jambo hilo kwa shukrani nyingi sana, ewe Mtukufu Feliksi. **4** Lakini ili nisitumie muda wako mwingi, ninakuomba kwa fadhili zako utusikilize kwa ufupi.

5 Kwa maana tumemwona mtu huyu kuwa msumbufu, ^e akichochea uasi ^f miongoni mwa Wayahudi wote katika dunia yote inayokaliwa, naye ni kiongozi wa madhehebu ya Wanazareti. ^g

6 Pia alijaribu kulichafua hekalu, basi tukamkamata. ^h

7 * — **8** Wewe mwenyewe

24:1 *Au “mwanasheria.” 24:5 *Tnn., “tauni.” 24:7 *Angalia Nyongeza A3.

utakapomhoji, utagundua mambo haya yote ambayo tunamshtaki.”

9 Ndipo Wayahudi pia wakajiunga katika shambulio hilo, wakisisitiza kwamba mambo hayo ni ya kweli. **10** Gavana alipomtolea Paulo ishara ili azungumze, akajibu:

“Ninajua vema kwamba ume-kuwa mwamuzi wa taifa hili kwa miaka mingi, nami nafurahi kujitetea mbele yako.^a

11 Unaweza kujihakikishia kwamba hazijapita zaidi ya siku 12 tangu nilipopanda kwenda kuabudu huko Yerusalemu.^b **12** nao hawakunipata hekaluni nikibishana na mtu yeyote wala kuchochea kikundi chenye ghasia, katika masinagogi au kotekote jijini.

13 Wala hawawezi kukuthibitisha mambo wanayonishtaki sasa hivi. **14** Lakini ninakiri jambo hili kwako, kwamba kulingana na njia wanayoiita ‘madhehebu,’ hivyo ndivyo ninavyomtolea utumishi mtakatifu Mungu wa mababu zangu,^c kwa kuwa ninaamini mambo yote yaliyo katika Sheria na yaliyoandikwa katika Manabii.^d **15** Nami nina tumaini kwa Mungu, tumaini ambalo watu hawa pia wanatazamia, kwamba kutakuwa na ufufuo^e wa waadilifu na wasio waadilifu pia.^f **16** Kwa sababu hiyo sikuzote ninajitahidi kudumisha dhamiri safi* mbele za Mungu na wanadamu.^g **17** Sasa baada ya miaka kadhaa, nilirudi ili kuleta zawadi za rehema^h kwa taifa langu na kutoa matoleo. **18** Nilipokuwa nikishughulikia mambo hayo, walinikuta

24:16 *Au “dhamiri isiyo na lawama.”

SURA YA 24

a Flp 1:7

b Mdo 21:17, 26

c Kut 3:15
Mdo 3:13
2Ti 1:3

d Mdo 28:23
Ro 3:21

e Isa 26:19
Mt 22:31, 32
Lu 14:13, 14
Yoh 5:28, 29
Yoh 11:25
Ebr 11:35
Ufu 20:12

f Lu 23:43

g Mdo 23:1
1Ko 4:4
Ebr 13:18

h 2Ko 8:4

Safu ya 2

a Mdo 21:24, 26

b Mdo 25:16

c Mdo 23:6

d Mdo 9:1, 2
Mdo 19:9

e Mt 10:18

f Mdo 17:30, 31
2Ko 5:10

hekaluni nikiwa nimetakaswa kisherehe,^a lakini sikuwa na umati wala sikuwa ninasababisha fujo. Lakini kulikuwa na Wayahudi fulani kutoka mkoa wa Asia **19** ambao wanapaswa kuwa hapa mbele yako ili wanishtaki ikiwa kwa kweli wana jambo lolote dhidi yangu.^b **20** Au uwaambie watu walio hapa waseme wenyewe kosa walilopata nilipokuwa nimesimama mbele ya Sanhedrini, **21** isipokuwa jambo hili moja nililosema kwa sauti kubwa nilipokuwa nimesimama kati yao: ‘Mimi ninahukumiwa leo mbele yenu kwa sababu ya ufufuo wa wafu!’^c

22 Hata hivyo, Feliksi, akiwa anajua vizuri ukweli kuhusu Njia hii,^d akaahirisha kesi yao kwa kusema: “Lisia kama nda wa jeshi atakapokuja, nitaamua mambo haya yanayowahusu.” **23** Naye akamwagiza ofisa wa jeshi kwamba mtu huyo awekwe chini ya kizuizi lakini apewe uhuru fulani, na watu wake waruhusiwe kumhudumia.

24 Siku kadhaa baadaye Feliksi akaja na Drusila mke wake, aliyekuwa Myahudi, akawatuma watu wamwite Paulo naye akamsikiliza akizungumza kuhusu imani katika Kristo Yesu.^e **25** Lakini Paulo alipokuwa akiongea kuhusu uadilifu na kujizuia* na hukumu itakayokuja,^f Feliksi akaogopa na kumwambia: “Kwa sasa unaweza kwenda, lakini nitakapopata nafasi nitakuita tena.” **26** Wakati huohuo alitumaini kwamba Paulo angempa pesa. Kwa hivyo, akamwita

24:25 *Au “kujidhibiti; kujiweza.”

mara nyingi na kuzungumza naye. **27** Lakini miaka miwili ilipokwisha, Porkio Festo alichukua nafasi ya Feliksi; na kwa sababu Feliksi alitamani kukubaliwa na Wayahudi,^a akamwacha Paulo akiwa amefungwa.

25 Kwa hiyo, baada ya Festo^b kufika katika mkoa na kuchukua mamlaka, siku tatu baadaye alipanda kwenda Yerusalemu kutoka Kaisaria. **2** Nao wakuu wa makuhani na watu mashuhuri kati ya Wayahudi wakamweleza mashtaka dhidi ya Paulo.^c Basi wakaanza kumwomba Festo **3** awaonyeshe kibali* kwa kumwita Paulo aje Yerusalemu. Lakini walikuwa wanapanga kumvizia Paulo na kumuua barabarani.^d **4** Hata hivyo, Festo akajibu kwamba Paulo alipaswa kuзуiliwa huko Kaisaria na kwamba baada ya muda mfupi yeye mwenyewe ange-rudi huko. **5** Akasema: “Basi wale walio na mamlaka kati yenu washuke pamoja nami na kumshtaki, ikiwa kwa kweli mtu huyu amefanya kosa lote.”^e

6 Kwa hiyo, baada ya kukaa kati yao siku zisizozidi nane au kumi, akashuka kwenda Kaisaria, na siku iliyofuata akaketi kwenye kiti cha hukumu na kuamuru Paulo aletwe. **7** Alipoingia, Wayahudi walio-kuwa wameshuka kutoka Yerusalemu wakasimama kumzunguka, wakitoa mashtaka mengi mazito ambayo hawakuweza kuyathibitisha.^f

8 Lakini Paulo akajitetea hivi: “Sijatenda dhambi yoyo-

SURA YA 24

a Mdo 25:9

SURA YA 25

b Mdo 24:27

c Mdo 24:1

d Mdo 23:20, 21

e Mdo 25:16

f Mt 5:11
Lu 23:1, 2
Mdo 24:5

Safu ya 2

a Mdo 24:11, 12

b Mdo 24:27

c Mdo 23:26, 29

d Mdo 28:17-19

e Mdo 25:2, 3

te dhidi ya Sheria ya Wayahu-di wala dhidi ya hekalu wala dhidi ya Kaisari.”^a **9** Festo akitamani kukubaliwa na Wayahudi,^b akamjibu Paulo: “Je, ungependa kupanda kwenda Yerusalemu ukahukumi-we huko mbele yangu kuhusu mambo haya?” **10** Lakini Paulo akasema: “Mimi nimesimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kaisari, ambapo ninapaswa kuhukumiwa. Sijawakosea Wayahudi, nawe pia umegundua jambo hilo. **11** Ikiwa, kwa kweli mimi ni mkosaji na nimefanya jambo lolote linalostahili kifo,^c niko tayari kufa; lakini kama mashtaka ya watu hawa hayana msingi, hakuna mtu aliye na haki ya kunikabidhi kwao ili tu apate kibali chao. Ninakata rufaa kwa Kaisari!”^d **12** Ndi-po Festo, baada ya kuzungumza na baraza la washauri, akajibu: “Umekata rufaa kwa Kaisari; nawe utaenda kwa Kaisari.”

13 Baada ya siku kadhaa, Agripa mfalme na Bernike wakafika Kaisaria kwa ajili ya ziara ya kumsalimia Festo. **14** Kwa kuwa wangekaa huko siku kadhaa, Festo akawasilisha kesi ya Paulo mbele ya mfalme, akisema:

“Kuna mwanamume ambaye Feliksi alimwacha akiwa mfungwa, **15** nami nilipokuwa Yerusalemu wakuu wa makuhani na wazee wa Wayahudi walileta habari kumhusu,^e wakiomba ahukumawe hatia.

16 Lakini nikawajibu kwamba si utaratibu wa Kiroma kumkabidhi mtu yeyote ili tu kupata kibali kabla ya mshtakiwa kukutana uso kwa uso

na wale waliomshtaki na kupata nafasi ya kujitetea kuhusu mashtaka.^a **17** Basi walipofika hapa, sikukawia, bali kesho yake niliketiki kwenye kiti cha hukumu na kuamuru mwanamume huyo aletwe. **18** Wale waliomshtaki waliposimama, hawakumshtaki kwa mambo maovu niliyotazamia.^b **19** Ila tu walikuwa wakibishana naye kuhusu ibada yao ya mungu^{*c} na kuhusu mtu fulani anayeitwa Yesu ambaye alikufa, lakini ambaye Paulo alikuwa akisisitiza kwamba yuko hai.^d **20** Sikujua jinsi ya kutatua mabishano haya, basi nikamuuliza kama angependa kwenda Yerusalemu ili akahukumiwe huko kuhusu mambo haya.^e **21** Lakini Paulo alipokata rufaa ili abaki kizuizi ni akisubiri uamuzi wa Augusto Mkuu,^{*f} nikaamuru azuiliwe mpaka nitakapomtuma kwa Kaisari.”

22 Ndipo Agripa akamwambia Festo: “Mimi mwenyewe ningependa kumsikia mtu huyo.”^g Akasema: “Kesho utamsikia.” **23** Basi kesho yake, Agripa na Bernike wakaja kwa fahari nyingi na kuingia katika ukumbi wa baraza pamoja na viongozi wa jeshi na vilevile wanaume mashuhuri wa jiji; naye Festo alipotoa amri, Paulo akaletwa. **24** Festo akasema: “Mfalme Agripa na nyote mlio hapa pamoja nasi, mnamwona mtu huyu ambaye Wayahudi wote wamenionamba huko Yerusalemu na huku pia, wakipaza sauti kwamba hapaswi kuendelea kuishi.^h **25** Lakini nikaona kwamba hakuwa ame-

25:19 *Au “dini yao.” 25:21 *Jina la cheo la maliki Mroma.

SURA YA 25

a Mdo 25:5

b Mdo 25:7

c Mdo 18:14, 15
Mdo 23:26, 29

d Mdo 22:6-8

e Mdo 25:9

f Mdo 25:11, 12

g Mdo 9:15

h Mdo 22:22

Safu ya 2

a Mdo 23:26, 29

SURA YA 26

b Mdo 25:13

c Mdo 24:5, 9

d Gal 1:13, 14

e Mdo 23:6
Flp 3:4, 5

f Mdo 22:3

g Mdo 24:15

fanya jambo lolote linalostahili kifo.^a Basi mtu huyu alipokata rufaa kwa Augusto Mkuu, niliamua kumpeleka. **26** Lakini sina jambo hususa la kumwandikia Bwana wangu kumhusu. Basi nimeleta mbele yenu nyote, na hasa mbele yako wewe, Mfalme Agripa, ili baada ya kumchunguza kihukumu, nipate jambo la kuandika. **27** Kwa maana ninaona haifai kumpeleka mfungwa bila kuonyesha mashtaka yanayomkabili.”

26 Agripa^b akamwambia Paulo: “Unaruhusiwa kujitetea.” Ndipo Paulo akanyoosha mkono wake na kuanza kujitetea:

2 “Kuhusu mambo yote ninayoshtakiwa na Wayahudi,^c Mfalme Agripa, ninafurahi kwamba ninajitetea mbele yako leo, **3** hasa kwa sababu wewe una ujuzi mwingi kuhusu desturi zote na vilevile mabishano kati ya Wayahudi. Kwa hiyo, ninakuomba unisikilize kwa subira.

4 “Kwa kweli, maisha niliyoishi tangu ujana miongoni mwa watu wangu^{*} na huko Yerusalemu yanajulikana vizuri na Wayahudi wote.^d **5** ambao mwanzoni walinifahamu, nao wakipenda wanaweza kutoa ushahidi kwamba niliishi nikiwa Farisayo^e kulingana na madhehebu yetu yenye msimamo mkali zaidi katika ibada yetu.^f **6** Lakini sasa, kwa sababu ya tumaini la ahadi iliyotolewa na Mungu kwa mababu zetu,^g nimeitwa kwenye hukumu; **7** makabila yetu 12 yanatumaini kuona ahadi hiyo ikitimizwa kwa kumtolea

26:4 *Au “taifa langu.”

Mungu utumishi mtakatifu kwa bidii usiku na mchana. Wayahudi wananishtaki kwa sababu ya tumaini hili,^a ewe Mfalme.

8 "Kwa nini mnafikiri* kwamba ni jambo lililowezezana kwa Mungu kuwafufua wafu?

9 Mimi niliamini kwamba ni-napaswa kufanya matendo mengi ili kulipinga jina la Yesu Mnzareti. **10** Hivyo ndivyo nilivyofanya huko Yerusalemu, niliwafunga gerezani wakatifu wengi,^b kwa maana nilikuwa nimepewa mamla-ka na wakuu wa makuhani;^c na walipopaswa kuuawa, nilipiga kura yangu dhidi yao. **11** Niliwaadhibu mara nyingi katika masinagogi yote, niki- jaribu kuwalazimisha waka- ne imani yao; na kwa saba- bu nilikuwa nimewakasirikia sana, nilifikia hatua ya kuwa- tesa hata katika majiji yaliyo mbali.

12 "Nilipokuwa nikifanya hivyo nikiwa safarini kwenda Damasko pia nikiwa na mam- laka na maagizo kutoka kwa wakuu wa makuhani, **13** katikati ya mchana nilio- na barabarani, ewe Mfalme, nuru kutoka mbinguni inayo- zidi mwangaza wa jua iki- mulika kunizunguka mimi na wale waliokuwa wakisafiri pa- moja nami.^d **14** Sisi sote tu- lipoanguka chini, nikasikia sauti ikiniambia katika lugha ya Kiebrania: 'Sauli, Sauli, kwa nini unanitesa? Kue- ndelea kuipiga teke micho- koo* kunafanya iwe vigumu kwako.' **15** Lakini nikauliza:

26:8 *Tnn., "mna hukumu." **26:14** *Mchokoo ni fimbo yenye ncha ili- yochongoka inayotumiwa kumwelekeza mnyama.

SURA YA 26
a Mdo 24:20, 21

b Yoh 16:2
Mdo 8:3
Iko 15:9
Gal 1:13
1Ti 1:13

c Mdo 9:1, 2, 14

d Mdo 9:3-5
Mdo 22:6-8

Safu ya 2

a Mdo 22:14, 15
Gal 1:11, 12
1Ti 1:12

b Mdo 22:21
Ro 11:13

c Isa 61:1

d Kol 1:13

e Yoh 8:12
2Ko 4:6

f Efe 2:1, 2

g 1Yo 3:5

h Mdo 9:22

i Mdo 9:28

j Mt 3:8

k Mdo 21:30, 31

l Lu 24:27, 44
Ro 3:21

m Zb 22:7
Zb 35:19
Isa 50:6
Isa 53:5

n Zb 16:10

o Zb 18:49
Isa 11:10
Lu 2:30-32

'Wewe ni nani Bwana?' Naye Bwana akajibu: 'Mimi ni Yesu, ambaye unamtesa. **16** Hata hivyo, inuka usimame kwa mi- guu yako. Kwa sababu nime- kutokea ili nikuchague uwe mtumishi na shahidi wa mambo ambayo umeona na pia mambo nitakayokuonye- sha kunihusu.^a **17** Nami ni- takuokoa kutoka kwa watu hawa na kutoka kwa mataifa ambayo ninakutuma kwao^b **18** ili kuwafungua macho,^c kuwageuza watoke gizani^d waingie kwenye nuru^e na wa- toke kwenye mamlaka ya She- tani^f wamgeukie Mungu, ili wasamehewe dhambi zao^g na kupata urithi miongoni mwa wale waliotakaswa kwa kunia- mini mimi.'

19 "Kwa hiyo, Mfalme Agri- pa, mimi sikukosa kutii ma- no hayo kutoka mbinguni, **20** lakini kwanza kwa wale walio huko Damasko^h kisha kwa wale walio Yerusalemu,ⁱ na katika nchi yote ya Yudea, na pia kwa mataifa, niliku- wa nikipeleka ujumbe kwa- mba wanapaswa kutubu na kumgeukia Mungu kwa ku- fanya matendo yanayoonye- sha toba.^j **21** Hiyo ndiyo sa- babu Wayahudi walinikama- ta hekaluni na kujaribu ku- niua.^k **22** Hata hivyo, kwa sababu nimepata msaada ku- toka kwa Mungu, mpaka leo hii ninaendelea kutoa usha- hidi kwa wadogo na wakubwa pia, bila kusema lolote zaidi ya yale ambayo Manabii na pia Musa walisema yatatukia^l— **23** kwamba Kristo atateseka^m na akiwa wa kwanza kufufu- lwa kutoka kwa wafu,ⁿ atawa- tangazia nuru watu hawa na pia mataifa."^o

24 Paulo alipokuwa akijite-tea kwa kusema mambo hayo, Festo akasema kwa sauti kubwa: “Unarukwa na akili, Paulo! Kusoma kwingi kunafanya urukwe na akili!” **25** Lakini Paulo akasema: “Mimi sirukwi na akili, ewe Mtukufu Festo, bali ninasema maneno ya kweli na ya akili timamu. **26** Kwa kweli, mfalme ninayezungumza naye kwa uhuru anajua vizuri mambo haya; nina hakika kwamba hakuna hata moja kati ya mambo haya ambalo hajui, kwa maana hakuna jambo lolote lililofanywa kisiri.^a **27** Je, wewe, Mfalme Agripa, unawaamini Manabii? Ninajua unawaamini.” **28** Lakini Agripa akamwambia Paulo: “Kwa muda mfupi ungenishawishi niwe Mkristo.” **29** Ndipo Paulo akasema: “Ninamwomba Mungu kwamba iwe ni kwa muda mfupi au muda mrefu, si wewe tu bali pia wote wanaonisikia leo wawe kama mimi nilivyo, ila tu bila vifungo hivi vya gereza.”

30 Ndipo mfalme akasimama, vilevile gavana na Bernike na watu walioketi pamoja nao. **31** Lakini walipokuwa wakiondoka wakaanza kua mbiana: “Mtu huyu hafanyi lolote linalostahili kifo au vifungo vya gereza.”^b **32** Kisha Agripa akamwambia Festo: “Mtu huyu angefunguliwa kama hangekuwa amekata ru-faa kwa Kaisari.”^c

27 Basi kwa kuwa iliamuliwa tusafiri baharini kwenda Italia,^d wakamkabidhi Paulo na wafungwa wengine kwa ofisa wa jeshi anayeitwa Yulio, wa kikosi cha Augusto.

SURA YA 26

a Yoh 18:20

b Mdo 23:26, 29
Mdo 25:24, 25

c Mdo 25:11, 12

SURA YA 27

d Mdo 25:12

Safu ya 2

a Mdo 19:29
Mdo 20:4
Kol 4:10b Law 16:29, 30
Law 23:27

2 Tukapanda meli kutoka Adramitiamu iliyokuwa karibu kusafiri kwenda kwenye bandari zilizo kando ya pwani za mkoa wa Asia, tukaa-nza safari; naye Aristarko^a Mmakedonia wa Thesalonike, alikuwa pamoja nasi. **3** Siku iliyofuata tukafika Sidoni, na Yulio akamtendea Paulo kwa fadhili* na kumruhusu aende kwa rafiki zake akatunzwe nao.

4 Tulipotoka huko, tukasafiri karibu na Kipro ili kujikinga na pepo zilizokuwa ziki-vuma kinyume nasi. **5** Kisha tukapita kwenye bahari kuu kandokando ya Kilikia na Pamfilia na kutia nanga kwenye bandari ya Mira huko Likia. **6** Huko ofisa wa jeshi akapata meli kutoka Aleksandria iliyokuwa ikielekea Italia, naye akatuagiza tupande meli hiyo. **7** Kisha baada ya kusafiri polepole kwa siku kadhaa, tukafika kwa shida huko Kinido. Kwa sababu upepo ulituzuia kusonga mbele, tukasafiri chini ya Krete karibu na Salmone. **8** Tukasafiri kwa shida kandokando ya pwani, tukafika mahali panapoitwa Bandari Nzuri, karibu na jiji la Lasea.

9 Muda mrefu ulikuwa ume-pita na kufikia sasa ilikuwa hatari kusafiri baharini, kwa sababu hata kipindi cha kufunga kwa Siku ya Kufunika Dhambi^b tayari kilikuwa kimepita, basi Paulo akatoa pendekezo, **10** akawaambia: “Ninaona kwamba safari hii itakuwa na madhara na hasara kubwa si kwa shehena na meli tu bali pia kwa uhai

27:3 * Au “fadhili za kibinadamu.”

wetu.”* **11** Hata hivyo, ofisa wa jeshi akamsikiliza nahodha na mwenye meli badala ya kusikiliza alichokuwa akisema Paulo. **12** Kwa kuwa bandari hiyo haikufaa wakati wa majira ya baridi kali, wengi wapakendekeza kuendelea na safari, ili kuona kama wangepaulu kukaa wakati wa majira ya baridi kali huko Feniki, ambayo ni bandari ya Krete inayofunguka kuelekea kaskazini mashariki na kuelekea kusini mashariki.

13 Upepo wa kusini ulipovuma kwa utulivu, walifikiri kwamba wametimiza kusemi lao, wakang’oa nanga na kuanza kusafiri kandokando ya Krete karibu na ufuo. **14** Hata hivyo, baada ya muda mfupi, upepo mkali unaoitwa Euroakilo* ukavuma kwa kasi juu yake. **15** Kwa kuwa meli ilipigwa na upepo wenyenguvu na ikashindwa kuukabili, tukaiachilia nao upepo ukatusukuma. **16** Kisha tukapita chini ya kisiwa kidogo kinachoitwa Kauda, na bado ilikuwa vigumu kuiokoa mashua ndogo* iliyokuwa kwenye tezi ya meli. **17** Lakini baada ya kuiingiza ndani, wakaifunga ile mashua kwenye meli, na kwa kuwa walio-gopa kukwama kwenye mchanga wa Sirti,* wakashusha vifaa vya kuendeshea na hivyo wakasukumwa na upepo. **18** Kwa sababu tulikuwa tukirushwarushwa kwa nguvu na dhoruba, siku iliyofuata wa-

27:10 *Au “nafsi zetu.” 27:14 *Yaani, upepo wa kaskazini mashariki. 27:16 *Mashua ndogo inayotumiwa kuokoa uhai. 27:17 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

Safu ya 2

SURA YA 27

a Mdo 27:9,10

b Mdo 5:18,19
Ebr 1:7,14

c Mdo 23:11
Mdo 25:11,12

d Mdo 28:1

kaanza kupunguza uzito wa meli. **19** Siku ya tatu, waka-tupa ayari za meli hiyo kwa mikono yao wenyewe.

20 Tulipokosa kuona jua wala nyota kwa siku nyingi na kupigwa na dhoruba kali,* mwishowe tulianza kupoteza tumaini la kuokoka. **21** Baada ya watu kukaa kwa muda mrefu bila kula, Paulo alisimama katikati yao na kusema: “Ikiwa mngefuata ushauri wangu hamngesafiri baharini kutoka Krete na hivyo hamngepatwa na madhara na hasara hii.” **22** Hata hivyo, sasa ninawahimiza mji-pe moyo, kwa maana hakuna hata mmoja wenu atakayopotea,* meli tu ndiyo itakayopotea. **23** Usiku huu malai-ka^b wa Mungu ambaye mimi ni mali yake na ambaye ninamtolea utumishi mtakatifu, alisimama kando yangu **24** akasema: ‘Usiogope, Paulo. Utasimama mbele ya Kaisari,^c na tazama! Mungu amekupa wale wote wanaosafiri pamoja nawe.’ **25** Basi jipeni moyo, kwa maana ninamwamini Mungu kwamba itakuwa kama nilivyoambiwa. **26** Hata hivyo, ni lazima tutupwe kwenye ufuo wa kisiwa fulani.”^d

27 Sasa usiku wa 14 ulipofika nasi tukawa tukirushwa huku na huku katika Bahari ya Adria, katikati ya usiku mabaharia walianza kuhisi kwamba walikuwa wakikaribia nchi kavu. **28** Wakapima kina kwa bildi na kupata pima 20,* basi wakasonga

27:20 *Tnn., “isiyo ndogo.” 27:22 *Au “nafsi itakayopotea.” 27:28 *Karibu mita 36 (futi 120). Angalia Nyongeza B14.

mbele kidogo wakapima tena na kupata pima 15.* **29** Wakiogopa kwamba tungekwa ma kwenye miamba, wakashusha nanga nne kutoka kwenye tezi na kuanza kutamani kupambazuke. **30** Lakini mabaharia walipojaribu kutoroka kutoka kwenye meli na kushusha mashua ndogo ndani ya bahari wakisingizia kwamba walikusudia kuzishusha nanga kutoka kwenye omo, **31** Paulo akamwambia ofisa wa jeshi na wanajeshi: "Watu hawa wasipobaki katika meli, ninyi hamwezi kuokoka."^a **32** Ndipo wanajeshi wakakata kamba za ile mashua ndogo na kuiacha ianguke.

33 Sasa kulipokaribia kupambazuka, Paulo akawahimiza wote wale chakula, akisema: "Kwa siku 14 mme kuwa mkisubiri kwa wasiwasi, bila kula chochote. **34** Basi ninawatia moyo mle chakula; kwa ajili ya usalama wenu, kwa maana hakuna hata unywele mmoja wa vichwa vyenu utakaopotea." **35** Baada ya kusema hivyo, akachukua mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote, akaumea, na kuanza kula. **36** Kwa hiyo wote wakajipa moyo, nao pia wakaanza kula. **37** Kwa ujumla, sote tulikuwa watu* 276 katika meli. **38** Walipokula chakula wakashiba, wakapunguza uzito wa meli kwa kutupa ngano baharini.^b

39 Kulipopambazuka, hawakuitambua nchi hiyo,^c lakini waliona ghuba yenye ufuo, nao waliazimia kuipeleka meli ufuoni kama wa-

27:28 *Karibu mita 27 (futi 90). Angalia Nyongeza B14. 27:37 *Au "nafsi."

SURA YA 27

a Mdo 27:22

b Yon 1:5

c Mdo 28:1

Safu ya 2

a Mdo 27:22
2Ko 11:25

b Mdo 27:23, 24

SURA YA 28

c Mdo 27:26

ngeweza. **40** Basi wakazikata nanga na kuziacha zianguke baharini, wakati huohuo wakifungua kamba za makasia ya usukani; na baada ya kutweka tanga la mbele kwenye upepo, wakaelekea ufuoni. **41** Wakagonga rundo kubwa la mchanga lililorundikwa na bahari pande zote, wakaendesha meli juu ya mchanga nayo omo ikakwama na kukaa bila kutikisika, lakini mawimbi yakaanza kuvunja tezi vipandevipande kwa nguvu.^a **42** Ndipo wanajeshi wakaamua kuwau wafungwa ili yeyote asiogelee na kutoroka. **43** Lakini ofisa wa jeshi alikuwa amezimia kumfikisha Paulo salama naye akawazuia ili wasitekeleze mpango wao. Akawaamuru wale ambao wangeweza kuogelea wajitupe baharini na watangulie kuogelea mpaka nchi kavu, **44** na wale wengine wangufuata, wengine wakiwa juu ya mbao na wengine juu ya vipande vya meli. Basi wote wakafika salama kwenye nchi kavu.^b

28 Tulipofika salama ufuoni, tukajua kwamba kisiwa hicho kiliitwa Malta.^c **2** Na watu hao waliozungumza lugha ya kigeni* walitute ndea kwa fadhili zinazopita za kawaida.[#] Wakawasha moto na kutakaribisha sote kwa fadhili kwa sababu mvua ilikuwa ikinyesha na kulikuwa na baridi. **3** Lakini Paulo alipokusanya tita la kuni na kuliweka juu ya moto, nyoka* akatoka kwa sababu ya joto na kujifunga kwenye mkono wake.

28:2 *Au "wenyeji wa nchi hiyo." [#]Au "fadhili za kibinadamu." 28:3 *Au "nyoka-kipiri."

4 Watu hao waliozungumza lugha ya kigeni walipomwona nyoka huyo mwenye sumu akining'inia kwenye mkono wake, wakaanza kuambiana: "Hakika mtu huyu ni muuaji, na ingawa alifika salama kutoka baharini, Haki* hai-kumruhusu aendelee kuishi." **5** Hata hivyo, akamkung'uta yule nyoka na kumtupa ndani ya moto, naye hakupatwa na madhara. **6** Lakini walitarajia kwamba atavimba au aanguke na kufa ghafla. Baada ya kusubiri kwa muda mrefu na kuona hajapatwa na jambo lolote baya, wakabadili maoni yao na kuanza kusema yeye ni mungu.

7 Sasa karibu na mahali hapo kulikuwa na mashamba ya mkuu wa kisiwa hicho, aliyetwa Publio, ambaye alitukaribisha na kutuonyesha ukarimu kwa siku tatu. **8** Ikawa kwamba baba ya Publio alikuwa amelala kitandani akiugua homa na ugonjwa wa kuhara damu. Paulo akaingia alimokuwa na kusali, akaweka mikono juu yake, akamponya.^a **9** Baada ya tukio hilo, wote waliokuwa wagonjwa katika kisiwa hicho wakaanza pia kuja kwake na kuponywa.^b **10** Pia wakatupatia zawadi nyingi, na tulipokuwa tukianza safari, wakapakia melini vitu vyote tulivyo-hitaji.

11 Miezi mitatu baadaye tukasafiri kwa meli ambayo upande wa mbele ilikuwa na sanamu ya "Wana wa Zeu." Meli hiyo ilitoka Aleksandria na ili-

28:4 *Neno la Kigiriki *Dí'ke*, ambalo huenda linarejelea mungu wa kike wa kulipiza kisasi au wazo la haki ya kudhaniwa.

SURA YA 28

a Lu 4:38, 39

b Mt 10:8

Safu ya 2

a 2Ko 1:3, 4

b Mdo 24:11, 12
Mdo 25:8

c Mdo 21:33

d Mdo 24:10

e Mdo 23:26, 29
Mdo 25:24, 25
Mdo 26:31, 32

f Mdo 25:11, 12

g Mdo 23:6
Mdo 26:6
Efe 6:19, 20
2Ti 1:16

kuwa imekaa kwenye kisiwa hicho wakati wa majira ya baridi kali. **12** Tukatia nanga katika bandari ya Sirakusa tukakaa huko siku tatu; **13** kutoka hapo tukasafiri mpaka Regiamu. Siku moja baadaye, upepo wa kusini ukaanza kuvuma nasi tukaingia Puteoli siku ya pili. **14** Tukawakuta akina ndugu huko, wakatusihi tukae pamoja nao kwa siku saba, kisha tukaelekea Roma. **15** Kutoka huko, akina ndugu waliposikia habari zetu, wakaja mpaka Soko la Apio na Mikahawa Mitatu ili kutupokea. Paulo alipowao-na, akamshukuru Mungu na kujipa moyo.^a **16** Mwishowe, tulipoingia Roma, Paulo aliruhusiwa kukaa peke yake akiwa na mwanajeshi aliyemlinda.

17 Hata hivyo, baada ya siku tatu akawaita wanaume mashuhuri wa Wayahudi. Walipokuwa wamekusanyika, akawaambia: "Wanaume, akina ndugu, ingawa sikuwa nimefanya jambo lolote kinyume cha watu au desturi za mababu zetu,^b nilikabidhiwa nikiwa mfungwa kutoka Yerusalemu na kutiwa mikononi mwa Waroma.^c **18** Na baada ya kufanya uchunguzi,^d walitaka kuniacha huru, kwa maana hawakuwa na sababu yoyote ya kuniua.^e **19** Lakini Wayahudi walipopinga, nililazimika kukata rufaa kwa Kaisari,^f lakini si kwa sababu nilikuwa na shtaka lolote dhidi ya taifa langu. **20** Basi kwa sababu hii niliomba kuwaona na kuzungumza nanyi, kwa maana nimefungwa mnyororo huu kwa sababu ya tumaini la Israel."^g **21** Wakamwambia: "Hautujapokea barua zozote kuku-

husu kutoka Yudea, wala hakuna ndugu yeyote aliyekuja kutoka huko ambaye ametujulisha au kusema jambo lote baya juu yako. **22** Lakini tunaona inafaa kusikia kutoka kwako maoni yako, kwa maana kwa kweli kuhusu madhehebu haya,^a tunajua yanasemwa vibaya kila mahali.”^b

23 Basi wakapanga siku ya kukutana pamoja naye, nao wakaja wakiwa wengi hata zaidi mahali alipoishi. Na kuanzia asubuhi mpaka jioni, akawafanulia jambo hilo na kutoa ushahidi kamili kuhusu Ufalme wa Mungu, ili kuwashawishi kumhusu Yesu^c kwa kutumia Sheria ya Musa^d na pia Manabii.^e **24** Baadhi yao wakaanza kuamini mambo aliyosema; lakini wengine hawakuamini. **25** Basi kwa sababu hawakukubaliana miongoni mwao, wakaanza kuondoka, naye Paulo akasema jambo hili moja:

“Kwa kufaa roho takatifu ili sema kupitia Isaya nabii kwa mababu zenu, **26** ikisema,

SURA YA 28

a Mdo 24:14

b Lu 2:34
Yoh 15:19

c Mdo 17:2, 3

d Yoh 5:46

e Mdo 26:22, 23

Safu ya 2

a Ro 11:8

b Isa 6:9, 10
Mt 13:14, 15c Lu 3:4, 6
Mdo 13:45, 46
Mdo 22:21
Ro 11:11d Zb 67:2
Zb 98:3
Isa 11:10

e Mdo 28:16

f Efe 6:19

‘Nenda kwa watu hawa uwaa-
mbie: “Kwa kweli mtasikia la-
kini hamtaelewa kamwe, na
kwa kweli mtatazama, lakini
hamtaona kamwe.”^a **27** Kwa
maana mioyo ya watu hawa
imekuwa migumu, nao wame-
sikia kwa masikio yao bila kui-
tikia, nao wamefunga macho
yao, ili wasione kamwe kwa
macho yao na kusikia kwa ma-
sikio yao na kuelewa kwa mio-
yo yao, nao wageuke nami ni-
waponye.”^b **28** Basi jueni
kwamba wokovu huu kutoka
kwa Mungu umepelekwa kwa
mataifa;^c nao kwa hakika wa-
tausikiliza.”^d **29** *—

30 Kwa hiyo akakaa huko
kwa miaka miwili kamili kati-
ka nyumba yake ya kukodi,^e
naye alikuwa akiwakaribisha
kwa fadhili wale wote walio-
mtembelea, **31** akiwahubiria
Ufalme wa Mungu na kuwafun-
disha kumhusu Bwana Yesu
Kristo kwa uhuru mwingi wa
kusema,^{*f} bila kizuizi.

28:29 *Angalia Nyongeza A3. **28:31**
*Au “kwa ujasiri wote.”

KWA

WAROMA

YALIYOMO

- 1 Salamu (1-7)
Paulo atamani kutembelea Roma (8-15)
Mwadilifu ataishi kupitia imani (16, 17)
Watu wasiomwogopa Mungu hawana
sababu ya kujitetea (18-32)
Sifa za Mungu zinaonekana kupitia
uumbaji (20)
- 2 Hukumu ya Mungu dhidi ya Wayahudi
na Wagiriki (1-16)

- Jinsi dhamiri inavyofanya kazi (14, 15)
Wayahudi na Sheria (17-24)
Kutahiriwa moyoni (25-29)
- 3 “Mungu na aonekane kuwa wa
kweli” (1-8)
Wayahudi na Wagiriki wako chini ya
dhambi (9-20)
Uadilifu kupitia imani (21-31)

- Wote wanapungukiwa na utukufu wa Mungu (23)
- 4 Abrahamu alitangazwa kuwa mwadilifu kupitia imani (1-12)
Abrahamu, baba ya wale walio na imani (11)
Kupokea ahadi kupitia imani (13-25)
- 5 Kupatanishwa na Mungu kupitia Kristo (1-11)
Kifo kupitia Adamu, uzima kupitia Kristo (12-21)
Dhambi na kifo vyaenea kwa wote (12)
Tendo moja la kutetewa (18)
- 6 Uhai mpya kupitia ubatizo katika Kristo (1-11)
Msiache dhambi itawale katika miili yenu (12-14)
Kuacha utumwa wa dhambi na kuwa watumwa wa Mungu (15-23)
Mshahara wa dhambi—kifo; Zawadi ya Mungu—uzima (23)
- 7 Kuwekwa huru kutoka Sheria kwafanuliwa (1-6)
Dhambi yafunuliwa kupitia Sheria (7-12)
Kupambana na dhambi (13-25)
- 8 Uzima na uhuru kupitia roho (1-11)
Roho ya kuwa wana hutoa ushahidi (12-17)
Uumbaji unangojewa uhuru wa wana wa Mungu (18-25)
'Roho hutuombea' (26, 27)
Mungu aliwachagua awali (28-30)
Ushindi kupitia upendo wa Mungu (31-39)
- 9 Paulo awahuzunikia Israeli wa kimwili (1-5)
Uzao wa kweli wa Abrahamu (6-13)
Mungu akichagua haiwezekani kumpinga (14-26)
- Vyombo vya ghadhabu na vya rehema (22, 23)
Ni mabaki tu watakaokolewa (27-29)
Israeli wajikwaa (30-33)
- 10 Jinsi ya kufikia uadilifu wa Mungu (1-15)
Tangazo la hadharani (10)
Kumwitia Yehova humaanisha wokovu (13)
Miguu ya wahubiri inapendeza (15)
Habari njema yakataliwa (16-21)
- 11 Israeli hawakukataliwa wote (1-16)
Mfano wa mzeituni (17-32)
Kina cha hekima ya Mungu (33-36)
- 12 Toeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai (1, 2)
Zawadi mbalimbali lakini mwili mmoja (3-8)
Ushauri kuhusu maisha ya Wakristo wa kweli (9-21)
- 13 Kujitiisha chini ya mamlaka (1-7)
Kulipa kodi (6, 7)
Upendo hutimiza Sheria (8-10)
Jiendesheni kama wakati wa mchana (11-14)
- 14 Msihukumiane (1-12)
Msiwakwaze wengine (13-18)
Jitahidi kupata amani na umoja (19-23)
- 15 Karibishaneni kama Kristo alivyofanya (1-13)
Paulo, mtumishi kwa mataifa (14-21)
Mipango ya safari za Paulo (22-33)
- 16 Paulo amtambulisha Fibi, mhudumu (1, 2)
Salamu kwa Wakristo huko Roma (3-16)
Waonywa kuhusu migawanyiko (17-20)
Salamu kutoka kwa wafanyakazi wenzi wa Paulo (21-24)
Siri takatifu yafunuliwa (25-27)

1 Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu aliyetwa awe mtume na kuwekwa kando kwa ajili ya habari njema ya Mungu,^a **2** ambayo aliahidi mapema kupitia manabii wake katika Maandiko matakatifu,

SURA YA 1

^a Mdo 9:11,15

Safu ya 2

^a 2Sa 7:8, 12

Lu 1:32

ZTi 2:8

^b Zb 2:7

Ebr 1:5

3 kuhusu Mwana wake, aliyetokana na uzao wa* Daudi^a kulingana na mwili, **4** lakini ambaye kwa nguvu alitangazwa kuwa Mwana wa Mungu^b kulingana na roho ya

1:3 *Tnn., "mbegu ya."

utakatifu kupitia ufufuo kutoka kwa wafu^a—ndiyo, Yesu Kristo Bwana wetu. **5** Kupitia yeye tulipokea fadhili zisizostahiliwa na utume^b ili watu wa mataifa yote^c wamtii na kuwa na imani na kulitukua jina lake, **6** ninyi pia mmeitwa kutoka kwa mataifa hayo ili muwe wa Yesu Kristo—**7** kwa ninyi nyote mlio huko Roma mkiwa wapendwa wa Mungu, walioitwa wawe watakatifu:

Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

8 Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu wangu kupitia Yesu Kristo kuwahusu ninyi nyote, kwa sababu imani yenu inazungumzwa ulimwenguni kote. **9** Kwa maana Mungu, ambaye ninamtolea utumishi mtakatifu kwa roho yangu kuhusiana na ile habari njema kuhusu Mwana wake, ni shahidi wangu wa jinsi ninavyowataja sikuzote katika sala zangu bila kuacha,^d **10** nikiomba kwamba ikiwezekana, hatimaye nifanikiwe kuja kwenu kwa mapenzi ya Mungu. **11** Kwa maana ninatamani kuwaona ninyi ili niwape zawadi ya kiroho kusudi mfanywe imara; **12** au badala yake, tutiane moyo,^e kila mmoja kupitia imani ya mwenzake, yenu na yangu pia.

13 Lakini, akina ndugu, sitaki mkose kujua kwamba mara nyingi nilikusudia kuja kwenu ili nipate matunda kati yenu pia kama ilivyo katika mataifa mengine, lakini nime-

1:12 *Au "kuwe na ubadilishanaji wa kitia moyo."

SURA YA 1

a Mdo 13:33

b 1Ti 2:7

c Mdo 15:14
Gal 2:7d 1Th 3:10
2Ti 1:3e 1Th 5:11
Ebr 10:25

Safu ya 2

a Mdo 19:21

b Mk 8:38
2Ti 1:8

c Ebr 11:6

d Mdo 3:25, 26

e Mdo 18:5, 6

f Yoh 3:36
Ro 3:21, 22g Hab 2:4
Gal 3:11
Ebr 10:38h Ro 2:5
Efe 5:6

i Ro 1:25

j Zb 19:1
Mdo 14:17k Isa 40:26
Ufu 4:11

l Yer 10:12

m Zb 103:19
Yer 10:10
Ufu 15:3

n Mwa 6:5

zuiwa mpaka sasa. **14** Mimi nina deni kwa Wagiriki na kwa watu wa mataifa ya kigeni,* kwa wenye hekima na wasio na akili pia: **15** kwa hiyo ninatamani kuwatangazia habari njema pia ninyi mlio huko Roma.^a **16** Kwa maana siionei aibu habari njema;^b kwa kweli, hiyo ni nguvu za Mungu kwa ajili ya wokovu kwa kila mtu aliye na imani,^c kwanza kwa Myahudi^d na pia kwa Mgiriki.^e **17** Kwa sababu kupitia habari njema, uadilifu wa Mungu unafunuliwa kupitia imani na kwa ajili ya imani,^f kama ilivyoandikwa: "Lakini mwadilifu ataishi kupitia imani."^g

18 Kwa kuwa ghadhabu ya Mungu^h inafunuliwa kutoka mbinguni dhidi ya watu wote wasiomwogopa Mungu na wasio waadilifu ambao wanaikandamiza kweliⁱ kwa njia isiyo ya uadilifu, **19** kwa sababu mambo yanayoweza kujulikana kuhusu Mungu yako wazi kabisa kati yao, kwa maana Mungu aliyaweka wazi kwao.^j

20 Kwa maana sifa zake zisizoonekana, zinaonekana waziwazi tangu kuumbwa kwa ulimwengu na kuendelea, kwa sababu zinaeleweka kupitia vitu vilivyombwa,^k yaani, nguvu zake za milele^l na Uungu,^m hivi kwamba hawana sababu ya kuji-tetea. **21** Kwa maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukua yeye akiwa Mungu wala hawakumshukuru, bali walikuwa wajinga katika fikira zao na moyo yao isiyo na ufahamu ikawa na giza.ⁿ

22 Ingawa walidai wana hekima, wakawa wapumbavu

1:14 *Au "wasio Wagiriki." Tnn., "wabaribari."

23 na kuugeza utukufu wa Mungu asiyeweza kuharibika kuwa kitu kama sanamu ya mwanadamu anayeweza kuharibika* na ya ndege na viumbe wenye miguu minne na viumbe wanaotambaa.^a

24 Kwa hiyo, kwa kupatana na tamaa za mioyo yao, Mungu aliwaacha katika uchafu, ili miili yao ivunjiwe heshima kati yao. **25** Waliibadili kweli ya Mungu kwa ajili ya uwongo, nao wakaabudu* uumbaji na kuutolea utumishi mtakati-fu badala ya kumtolea Muumba, anayesifiwa milele. Amina. **26** Ndiyo sababu Mungu aliwaacha katika hamu yenye kufedhehesha ya ngono,^b kwa maana wanawake wao walibadili matumizi yao ya asili kuwa kinyume cha asili;^c **27** vivyo hivyo pia wanaume waliacha matumizi ya asili ya* mwanamke na kuwakiana tamaa kali za uchu wao kwa wao, wanaume kwa wanaume,^d wakitenda mambo machafu na kupokea ndani yao wenyewe adhabu^e kamili, kwa sababu ya kosa lao.^e

28 Kwa sababu waliona hai-fai kumkubali Mungu,* Mungu aliwaacha katika hali ya akili isiyokubalika, ili wafanye mambo yasiyofaa.^f **29** Nao wakajaa kila namna ya ukosefu wa uadilifu,^g uovu, pupa,^h na ubaya, wakiwa wamejaa wivu,ⁱ uuaji,^j mizozo, udanganyifu,^k na nia ya kuwaumiza wengine,^l wakiwa wanong'onezaji,^m **30** wasenge-

1:23 *Au "kufa." 1:25 *Au "wakaushimu sana." 1:27 *Au "mahusiano ya asili pamoja na." #Au "malipo." 1:28 *Au "hawakukubali kumjua Mungu katika ujuzi sahihi." 1:29 *Au "tamaa mba-ya." #Au "wadaku; wambeya."

SURA YA 1

a Yer 2:11
Mdo 17:29

b Gal 5:19
1Th 4:4, 5

c Yud 7

d Mwa 19:5
Law 18:22
Law 20:13
1Ko 6:9, 10

e Gal 6:7

f Gal 5:19-21

g 1Pe 4:3

h Kum 5:21

i Tit 3:3

j 1Yo 3:15

k 1Pe 2:1

l Efe 4:31

Safu ya 2

a 1Pe 2:1

b Kum 21:18, 21

c Ro 1:21

d Ufu 21:8

SURA YA 2

e Ro 2:9

f Mt 7:5

g Ro 11:22
Efe 1:7

h Ro 3:25

i Isa 30:18

j 2Pe 3:9

k 2Th 1:7, 8
Ufu 6:16, 17
Ufu 11:18

nyaji,^a wenye kumchukia Mungu, wenye dharau, wenye majivuno, wenye kujidai, wenye kutunga mambo mabaya,* wasiotii wazazi.^b **31** wasio na uelewaji,^c wanaovunja makubaliano, wasio na upe-ndo wa asili, na wasio na rehma. **32** Ingawa wanajua vizuri amri ya uadilifu ya Mungu—kwamba wale wanaozoea kufanya mambo kama hayo wanastahili kifo^d—wanaendelea kuyafanya na pia wanakubaliana na wale wanaozoea kuyafanya.

2 Kwa hiyo huwezi kujitetea, ewe mwanadamu, hata uwe nani,^e ikiwa unahukumu; kwa maana unapomhukumu mwingine, unajihukumu wewe mwenyewe, kwa sababu wewe unayehukumu umezoea kufanya mambo hayo. **2** Sasa tunajua kwamba, hukumu ya Mungu inapatana na kweli, dhidi ya wale wanaozoea kufanya mambo hayo.

3 Lakini ewe mwanadamu, unadhani utaponyoka hukumu ya Mungu unapowahukumu wale wanaozoea kufanya mambo hayo na bado wewe unayafanya? **4** Au je, wewe unadharau utajiri wa fadhili zake^g na uvumilivu^{*h} na subira,ⁱ kwa sababu hujui kwamba Mungu kwa fadhili zake anajaribu kukuongoza wewe kwenye toba?^j **5** Lakini kulingana na ukaidi wako na moyo wako usiotubu, unajiwekea akiba ya ghadhabu katika siku ya ghadhabu na ya kufunuliwa kwa hukumu ya uadilifu ya Mungu.^k **6** Naye atamlipa kila mmoja kulingana na

1:30 *Au "yenye kudhuru." 2:4 *Au "ustahimilivu."

matendo yake:^a **7** uzima wa milele kwa wale wanaotafuta utukufu na heshima na kutoharibika,^b kwa uvumilivu katika kazi iliyo njema; **8** hata hivyo, kwa wale wenye ugomvi na wale wasioitii kweli lakini wanatii ukosefu wa uadilifu, kutakuwa na ghadhabu na hasira.^c **9** Kutakuwa na dhiki na taabu kwa kila mtu* anayefanya mabaya, kwanza kwa Myahudi na pia kwa Mgiriki; **10** bali utukufu na heshima na amani kwa kila mtu anayefanya mema, kwanza kwa Myahudi^d na pia kwa Mgiriki.^e **11** Kwa maana Mungu hana ubaguzi.^f

12 Kwa kuwa wote waliofanya dhambi bila sheria wataangamia pia bila sheria;^g bali wote waliofanya dhambi chini ya sheria watahukumiwa kwa sheria.^h **13** Kwa maana wale wanaosikia sheria sio waadilifu mbele za Mungu, bali wale wanaoshika sheria watatangazwa kuwa waadilifu.ⁱ **14** Kwa maana watu wa mataifa wasio na sheria^j wanapofanya kwa asili mambo ya sheria, watu hawa, ingawa hawana sheria, wao ni sheria kwao wenyewe. **15** Wao wenyewe wanaonyesha kuwa yaliyomo katika sheria yameandikwa ndani ya miyo yao, huku dhalmiri yao ikiwatolea ushahidi, na kwa* fikira zao wenyewe wanashtakiwa au hata kutetewa. **16** Hili litatendeka siku ambayo Mungu kupitia Kristo Yesu atahukumua mambo ya siri ya wanadamu,^k kulingana na habari njema ninayoita-ngaza.

2:9 *Au "nafsi ya kila mtu." 2:15 *Tnn., "katikati ya."

SURA YA 2

a Zb 62:12
Met 24:12
Mt 16:27

b 1Ko 15:53
Ufu 20:6

c Ro 1:18
Kol 3:6
Ebr 10:26, 27

d Yoh 4:22
Mdo 13:45, 46

e Mdo 15:14

f Kum 10:17
2Nya 19:7
Mdo 10:34, 35

g Efe 2:12

h Ro 3:19

i Kum 30:14
Eze 20:11
Yak 1:22

j Zb 147:19, 20

k Yoh 5:22
Mdo 10:42
1Pe 4:5

Safu ya 2

a Ro 9:6

b Kum 4:8

c Mt 23:2, 3

d Kut 20:15

e Kum 5:18

f Isa 52:5
Eze 36:20

g Mwa 17:10

h 1Ko 7:19
Gal 5:3

i Efe 2:11

j Ro 4:9, 10

17 Sasa, ikiwa wewe ni Myahudi kwa jina^a na unategemea sheria na kujivunia Mungu, **18** na unajua mapeenzi yake na unakubali mambo yaliyo bora kabisa kwa sababu unafundishwa* kutokana na Sheria,^b **19** nawe unasadiki kwamba wewe ni kiongozi wa vipofu, nuru kwa walio gizani, **20** mrekebishaji wa wale wasio na akili, mwaliimu wa watoto wadogo, na una picha ya ujuzi na ya ile kweli katika Sheria— **21** hata hivyo, je, wewe unayefundisha mtu mwingine, hujifundishi mwenyewe?^c Wewe unayehubiri, "Usiibe,"^d je, wewe huiba? **22** Wewe unayesema, "Usifanye uzinzi,"^e je, wewe hufanya uzinzi? Wewe unayechukia sanamu, je, wewe huiba katika mahekalu? **23** Wewe unayejivunia sheria, je, unamvunjia Mungu heshima kwa kuivunja Sheria? **24** Kwa maana "watu wanalikufuru jina la Mungu miongoni mwa mataifa kwa sababu yenu," kama ilivyoandikwa.^f

25 Kwa kweli, kutahiriwa^g kuna faida ikiwa tu umezoea kuifuata sheria;^h lakini ikiwa wewe huvunja sheria, kutahiriwa kwako kumekuwa kutahiriwa. **26** Kwa hiyo, ikiwa mtu asiyetahiriwaⁱ huyashika matakwa ya uadilifu ya Sheria, kutotahiriwa kwake kutahesabiwa kuwa kutahiriwa, si-vyo?^j **27** Na mtu asiyetahiriwa kimwili, akiishika Sheria, atakuhukumua wewe ambaye huvunja sheria ingawa una sheria zilizoandikwa na ume-tahiriwa. **28** Kwa kuwa yeye si Myahudi aliye hivyo kwa

2:18 *Au "unafundishwa kwa mdomo."

nje,^a wala kutahiriwa si kitu kilicho nje, juu ya mwili.^b **29** Bali yeye ni Myahudi aliye hivyo kwa ndani,^c na kutahiriwa kwake ni kule kwa moyo^d kupitia roho, wala si kupitia sheria zilizoandikwa.^e Sifa ya mtu huyo hutoka kwa Mungu, si kwa wanadamu.^f

3 Basi, Myahudi ana ubora gani, au kutahiriwa kuna faida gani? **2** Ni nyingi katika kila njia. Kwanza kabisa, wao walikabidhiwa maneno matakatifu ya Mungu.^g **3** Basi, hali ikoje? Ikiwa wengine walikosa imani, je, ukosefu wao wa imani utaondoa uaminifu wa Mungu? **4** La hash! Bali Mungu na aonekane kuwa wa kweli,^h hata ikiwa kila wanadamu ataonekana kuwa mwongo,ⁱ kama ilivyoandikwa: "Ili uthibitike kuwa mwadilifu katika maneno yako na ushinde wakati unapohukumiwa."^j **5** Hata hivyo, ikiwa ukosefu wetu wa uadilifu unaonyesha wazi uadilifu wa Mungu, tuseme nini? Mungu hakosi kutenda kwa haki anapoonyesha ghadhabu yake, sivyo? (Ninaongea kama mwanadamu.) **6** Hapana! Ikiwa hivyo, Mungu atauhukumu ulimwengu jinsi gani?^k

7 Lakini ikiwa kupitia uwongo wangu kweli ya Mungu imeonekana wazi zaidi kwa utukufu wake, kwa nini mimi pia ninahukumiwa kuwa mtena dhambi? **8** Na kwa nini tusiseme, kama watu fulani wanavyodai kwa uwongo kwamba tunasema, "Tufanye mambo mabaya ili mambo mema yaje"? Hukumu dhidi ya watu hao inapatana na haki.^l

9 Tuseme nini basi? Je, sisi tuna hali bora zaidi? Si-

SURA YA 2

a Yoh 8:39
Ufu 2:9

b 1Ko 7:19

c Ro 9:6

d Yer 4:4
Mdo 7:51
Flp 3:3

e Ro 7:6

f Yoh 5:44
1Ko 4:5

SURA YA 3

g Kum 4:8
Zb 147:19, 20
Mdo 7:38

h Isa 55:10, 11
Yoh 8:26
ZTi 2:13

i Hes 23:19
Zb 116:11

j Zb 51:4

k Zb 9:8
Zb 96:13
Zb 98:9
Mdo 17:31

l Ebr 2:2, 3

Safu ya 2

a Ro 3:23
Gal 3:22

b Met 20:9
Mhu 7:20

c Zb 14:1-3

d Zb 5:9

e Zb 140:3

f Zb 10:7
Yak 3:8, 9

g Met 1:16

h Isa 59:7, 8

i Zb 36:1

j Ro 2:12
Ro 5:13
Gal 3:10

k Gal 2:16
Gal 3:11

l Ro 7:9, 13
Gal 3:19

m Ro 1:16, 17

n Isa 53:11
Yer 31:34
Da 9:24

vyo hata kidogo! Kwa maana hapo juu tumefanya shtaka kwamba Wayahudi na vilevile Wagiriki wote wako chini ya dhambi;^a **10** kama ilivyoandikwa: "Hakuna mwanadamu mwadilifu, hakuna hata mmoja;^b **11** hakuna yeyote aliye na ufahamu; hakuna yeyote anayemtafuta Mungu. **12** Watu wote wamegeuka kando, wote wamekuwa wasiofaa kitu; hakuna yeyote anayetenda kwa fadhili, hakuna hata mmoja."^c **13** "Koo lao ni kaburi lililo wazi, wamedanganya kwa ndimi zao."^d "Sumu ya nyoka iko nyuma ya midomo yao."^e **14** "Na kinywa chao kimejaa kulaani na uchungu."^f **15** "Miguu yao inaharakisha kwenda kumwaga damu."^g **16** "Njia zao zina uharibifu na maumivu, **17** nao hawajaijua njia ya amani."^h **18** "Hakuna hofu ya Mungu mbele ya macho yao."ⁱ

19 Sasa tunajua kwamba mambo yote ambayo Sheria inasema, inawaambia wale walio chini ya Sheria, ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote ustahili adhabu kutoka kwa Mungu.^j **20** Kwa hiyo, hakuna mtu yeyote atakayetangazwa* kuwa mwadilifu mbele zake kupitia mateendo ya sheria,^k kwa maana kupitia sheria tunapata ujuzi sahihi kuhusu dhambi.^l

21 Lakini sasa uadilifu wa Mungu umefunuliwa bila sheria,^m kama inavyoshuhudiwa na Sheria na Manabii,ⁿ **22** ndiyo, uadilifu wa Mungu kupitia imani katika Yesu Kristo, kwa wote walio na ima-

3:20 *Tnn., "mwili wowote utakaotan-gazwa."

ni. Kwa maana hakuna tofauti.^a **23** Kwa maana wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,^b **24** nayo ni zawadi ya bure^c kwamba wanatangazwa kuwa waadilifu kwa fadhili zake zisizostahiliwa^d kupitia kuachiliwa huru kwa njia ya fidia ambayo Kristo Yesu alilipa.^e **25** Mungu alimtoa kuwa dhambi ya upatanisho^{*f} kupitia imani katika damu yake.^g Ilikuwa hivyo ili kuonyesha uadilifu wake mwenyewe, kwa sababu Mungu kwa uvumilivu^h wake alikuwa akizisamehe dhambi zilizofanywa wakati uliopita. **26** Ilikuwa hivyo ili kuonyesha uadilifu wake^h katika majira haya, ili awe mwadilifu hata anapomtanga za kuwa mwadilifu mtu aliyen a imani katika Yesu.ⁱ

27 Basi, je, tuna sababu ya kujisifu? Hatuna sababu. Kupitia sheria gani? Ile ya matendo?^j Hapana, bali kupitia sheria ya imani. **28** Kwa maana tunajua kwamba mtu hutangazwa kuwa mwadilifu kwa imani bila matendo ya sheria.^k **29** Au je, yeye ni Mungu wa Wayahudi peke yao?^l Je, yeye si Mungu wa watu wa mataifa pia?^m Ndiyo, pia wa watu wa mataifa.ⁿ **30** Kwa kuwa Mungu ni mmoja,^o atawatangaza watu waliotahiriwa kuwa waadilifu^p kutokana na imani na watu wasiotahiriwa kuwa waadilifu^q kupitia imani yao. **31** Basi, je, tunaifuta sheria kupitia imani yetu? La hasha! Badala yake, tunaiunga mkono sheria.^r

3:25 *Au "dhambi hu kufunika dhambi."
^aAu "ustahimilivu."

SURA YA 3

a Gal 3:28

b Mhu 7:20

c Ro 5:17

d Efe 2:8

e Mt 20:28

1Ti 2:5, 6

1Pe 2:24

f Isa 53:11

2Ko 5:19

1Yo 2:1, 2

1Yo 4:10

g Law 17:11

Mdo 13:39

Efe 1:7

h Zb 89:14

i 1Ko 1:30

1Yo 1:9

j Mdo 13:38, 39

Efe 2:8, 9

k Gal 2:15, 16

Yak 2:24

l Mdo 17:26, 27

m Mdo 10:4

n Isa 54:5

Ro 10:12

Gal 3:14

o Kum 6:4

1Ko 8:6

Efe 4:6

p 1Ko 7:18

q Gal 3:8

r Mt 5:17

Ro 8:3, 4

Ro 13:10

Safu ya 2

SURA YA 4

a Mwa 15:6

Gal 3:6

Yak 2:23

b Gal 2:15, 16

c Zb 32:1, 2

d Ro 3:30

e Ro 4:3

f Mwa 17:1, 2, 11

4 Ikiwa ni hivyo, tutase-
 ma alipata faida gani Abrahamu, babu yetu kulingana na mwili? **2** Kwa mfano, ikiwa Abrahamu alitangazwa kuwa mwadilifu kwa sababu ya matendo, angekuwa na sababu ya kujisifu, lakini si mbele za Mungu. **3** Kwani andiko linasema nini? "Abrahamu alikuwa na imani katika Yehova,* na hilo likahesabiwa kwake kuwa uadilifu."^a **4** Basi kwa mtu anayefanya kazi, malipo yake hayahesabiwi kuwa fadhili zisizostahiliwa bali ni deni. **5** Kwa upande mwingine, mtu asiyefanya kazi bali anaweka imani katika Yule anayemtangaza kuwa mwadilifu mtu asiyemwogopa Mungu, imani yake inahesabiwa kuwa ni uadilifu.^b **6** Kama vile Daudi pia anavyosema kuhusu furaha ya mtu ambaye Mungu humhesabu kuwa mwadilifu bila matendo: **7** "Wenye furaha ni wale ambao matendo yao ya kuasi sheria yamesamehewa na ambao dhambi zao zimefunikwa;* **8** mwenye furaha ni mtu ambaye Yehova* hatahesabu dhambi yake kamwe."^c

9 Basi, je, furaha hiyo huja tu kwa watu waliotahiriwa au pia kwa watu wasiotahiriwa?^d Kwa maana tunasema: "Imani ya Abrahamu ilihesabiwa kwake kuwa uadilifu."^e **10** Basi, ilihesabiwa kuwa uadilifu chini ya hali gani? Ali-pokuwa ametahiriwa au kabla ya kutahiriwa? Ni kabla ya kutahiriwa. **11** Naye alipokea ishara^f—yaani, kutahiriwa—kuwa muhuri wa* uadilifu

4:3, 8 *Angalia Nyongeza A5. 4:7 *Au "zimesamehewa." 4:11 *Au "dhamana ya; uhakikisho wa."

kwa imani aliyokuwa nayo alipokuwa katika hali yake ya kutotahiriwa, ili awe baba ya wale wote walio na imani^a ingawa hawajatahiriwa, kusiidi wahesabiye kuwa waadilifu; **12** na ili awe baba ya uzao uliotahiriwa, si kwa wale tu wanaoshikamana na kutahiriwa, bali pia kwa wale wanaotembea kwa utaratibu katika hatua za imani ambayo baba yetu Abrahamu^b alikuwa nayo katika hali ya kutotahiriwa.

13 Kwa maana Abrahamu au uzao wake* hawakupata ahadi kwamba atakuwa mriti wa ulimwengu kupitia sheria,^c bali kupitia uadilifu kwa imani.^d **14** Kwa maana ikiwa wale wanaoshika sheria ni warithi, imani inakuwa isiyofaa kitu na ahadi imefutwa. **15** Kwa kweli Sheria hutokeza ghadhabu,^e lakini pasipo na sheria, hakuna kosa lolote.^f

16 Ndiyo sababu ni kupitia imani, ili iwe kulingana na fadhili zisizostahiliwa,^g kusiidi ahadi iwe hakika kwa uzao wake* wote,^h si kwa wale tu wanaoshika Sheria, bali pia kwa wale wanaoshika imani ya Abrahamu, ambaye ni baba yetu sote.ⁱ **17** (Kama tu ilivyoandikwa: "Nimekuweka uwe baba ya mataifa mengi.") Hili lilikuwa machoni pa Mungu, ambaye Abrahamu alimwamini, anayewafanya wafu kuwa hai na kuyaita mambo yasiyokuwako kana kwamba yako.* **18** Ingawa hakukuwa na tumaini, lakini kwa kutegemea tumaini, alikuwa na imani kwamba angekuwa baba ya

4:13, 16 *Tnn., "mbegu yake." 4:17 *Au labda, "anafanya vitu visivyokuwapo viwepo."

SURA YA 4

a Ro 4:16

Gal 3:7

b Gal 3:29

c Mwa 12:1-3

Mwa 17:5, 6

Mwa 22:17, 18

d Ebr 11:8

e Ro 3:20

Ro 5:20

2Ko 3:7

f Ro 5:13

g Ro 3:24

h Ro 9:8

Gal 3:29

i Ro 4:11

j Mwa 17:5

Safu ya 2

a Mwa 15:5

Ebr 11:17, 18

b Mwa 17:17

c Mwa 18:11

Ebr 11:11, 12

d Ebr 11:19

e Mwa 15:6

Yak 2:23

f Ro 15:4

g Mdo 2:24

Mdo 13:30

1Pe 1:21

h Mt 20:28

i Isa 53:11, 12

2Ko 5:21

SURA YA 5

j Mdo 13:38, 39

k Efe 2:14

l 2Ko 5:18

Efe 3:11, 12

Ebr 10:19

mataifa mengi kulingana na yale yaliyokuwa yamesemwa: "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako."*^a **19** Na ingawa imani yake haikudhoofika, alifikiria mwili wake mwenyewe, sasa ukiwa kama tayari umekufa (kwa kuwa alikuwa na umri wa karibu miaka 100),^b na pia hali ya kufa* ya tumbo la uzazi la Sara.^c **20** Lakini kwa sababu ya ahadi ya Mungu, yeye hakusitasita kwa kukosa imani; bali alikuwa mwenye nguvu kwa imani yake, akiempa Mungu utukufu **21** na akiwa na uhakika kamili kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kutimiza kile alichohidi.^d **22** Kwa hiyo "ikahesabiwa kwake kuwa uadilifu."^e

23 Hata hivyo, maneno "lihesabiwa kwake" hayakuandikwa kwa ajili yake tu,^f **24** bali pia kwa ajili yetu ambao itahesabiwa, kwa sababu tunamwamini Yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu kutoka kwa wafu.^g **25** Alitolewa kwa ajili ya makosa yetu^h na kufufuliwa kwa ajili ya kututangaza sisi kuwa waadilifu.ⁱ

5 Basi, kwa kuwa sasa tumetangazwa kuwa waadilifu kutokana na imani,^j na tufurahie amani* pamoja na Mungu kupitia Bwana wetu Yesu Kristo,^k **2** ambaye kupitia kwake sisi pia tumepata fursa ya kuingia kwa imani katika fadhili hizi zisizostahiliwa ambamo sasa tunasimama;^l na tushangilie,* kwa kutegemea tumaini la utukufu wa Mungu. **3** Si hilo tu,

4:18 *Tnn., "mbegu yako." 4:19 *Au "hali ya kuwa tasa." 5:1 *Au labda, "tuna amani." 5:2 *Au labda, "tunashangilia."

bali na tushangilie* tukiwa katika dhiki,^a kwa kuwa tunajua kwamba dhiki hutokeza uvumilivu;^b **4** nao uvumilivu, hali yenye kukubaliwa;^c nayo hali yenye kukubaliwa, tumaini,^d **5** nalo tumaini halikatishi tamaa;^e kwa sababu upendo wa Mungu umemimnina ndani ya mioyo yetu kupitia roho takatifu, ambayo tulipewa.^f

6 Kwa maana, kwa kweli, tulipokuwa bado dhaifu,^g Kristo alikufa wakati uliowekwa kwa ajili ya watu wasiomwogopa Mungu. **7** Kwa maana ni vigumu kwa yeyote kufa kwa ajili ya mtu mwadilifu; hata hivyo labda mtu anaweza kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. **8** Lakini Mungu hupendekeza upendo wake kwetu kwa kuwa tulipokuwa bado watenda dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.^h **9** Kwa kuwa sasa tumetangazwa kuwa waadilifu kwa damu yake,ⁱ tutaokolewa hata zaidi kutokana na ghadhabu kupitia yeye.^j **10** Kwa maana, ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kupitia kifo cha Mwana wake,^k tutaokolewa hata zaidi kwa uhai wake, kwa kuwa sasa tumepatanishwa. **11** Si hilo tu, bali pia tunashangilia katika Mungu kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kupitia kwake sasa tumepokea upatanisho.^l

12 Hiyo ndiyo sababu, kama vile kupitia mtu mmoja dhambi iliingia katika ulimwengu na kifo kupitia dhambi,^m basi kifo kikaenea kwa watu wote kwa sababu wote walikuwa wamefanya dhambiⁿ—. **13** Kwa maana dhambi iliku-

SURA YA 5

- a Flp 2:17
1Pe 4:12,13
b Mdo 5:41,42
c Yak 1:12
d Flp 1:18-20
e Yos 21:45
f 2Ko 1:22
Gal 4:6
Efe 1:13,14
g Efe 2:1,5
h Isa 53:12
Yoh 3:16
Efe 2:4,5
1Pe 3:18
1Yo 4:10
i Mdo 13:38,39
Ebr 9:14
j 1Th 1:10
k 2Ko 5:18
Kol 1:21,22
l 2Ko 5:19
m Mwa 2:17
Mwa 3:6
Mwa 3:19
1Ko 15:21
n Zb 5:15
Ro 3:23

Safu ya 2

- a Ro 4:15
b 1Ko 15:45
c Ebr 2:9
d Isa 53:11
Mt 20:28
e Mwa 2:17
Mwa 3:6
f Mwa 3:17-19
g Ro 4:25
h Ro 5:12,14
i Ro 3:24
j Ufu 5:9,10
Ufu 20:4
k 1Pe 3:18
Ufu 1:5,6
l 1Ko 15:21
m Ro 1:16
1Ti 2:3,4
n Yoh 10:10

wa katika ulimwengu kabla ya Sheria, lakini mtu yeyote hahesabiwi kuwa na dhambi ikiwa hakuna sheria.^a **14** Hata hivyo, kifo kilitawala kama mfalme tangu Adamu mpaka Musa, hata juu ya wale ambao hawakuwa wamefanya dhambi kama vile Adamu alivyofanya kosa, ambaye ni mfano wa yule aliyepaswa kuja.^b

15 Lakini zawadi si kama lile kosa. Kwa maana ikiwa kwa kosa la mtu mmoja wengi walikufa, fadhili zisizostahiliwa za Mungu na zawadi yake ya bure kupitia fadhili zisizostahiliwa za mtu mmoja,^c Yesu Kristo, zilizidi* hata zaidi kwa wengi!^d **16** Pia, ile zawadi ya bure si sawa na jinsi mambo yalivyotendeka kupitia mtu mmoja aliyefanya dhambi.^e Kwa maana hukumu baada ya kosa moja ilikuwa hatia,^f lakini zawadi baada ya makosa mengi ilikuwa tangazo la uadilifu.^g **17** Kwa maana ikiwa kwa kosa la mtu mmoja kifo kilitawala kama mfalme kupitia mtu huyo,^h wale wanaopokea wingi wa fadhili zisizostahiliwa na zawadi ya bure ya uadilifuⁱ watatawala hata zaidi wakiwa wafalme^j katika uzima kupitia mtu mmoja, Yesu Kristo!^k

18 Kwa hiyo basi, kama vile kupitia kosa moja matokeo kwa watu wa namna zote yalikuwa kuhukumiwa hatia,^l vi- vyo hivyo kupitia tendo moja la kutetewa matokeo kwa watu wa namna zote^m ni wao kutangazwa kuwa waadilifu kwa ajili ya uzima.ⁿ **19** Kwa maana kama vile kupitia kutotii kwa mtu mmoja wengi walifanywa kuwa watenda

5:3 *Au labda, "tunashangilia."

5:15 *Au "zilifurika."

dhambi,^a vivyo hivyo pia kupitia kutii kwa mtu mmoja wengi watafanywa kuwa waadilifu.^b **20** Basi Sheria ilikuja ili makosa yaongezeke.^c Lakini mahali ambapo dhambi ilizidi, fadhili zisizostahiliwa zilizidi hata zaidi. **21** Kwa kusudi gani? Ili kama vile dhambi ilivyotawala kama mfalme pamoja na kifo,^d vivyo hivyo pia fadhili zisizostahiliwa zitawale kama mfalme kupitia uadilifu na kuleta uzima wa milele kupitia Yesu Kristo Bwana wetu.^e

6 Basi tuseme nini? Je, tundelee kuwa katika dhambi, ili fadhili zisizostahiliwa ziongezeke? **2** La hash! Kwa kuwa tulikufa kuhusiana na dhambi,^f tunawezaje kuendelea kuishi tena katika dhambi?^g **3** Au je, hamjui kwamba sisi sote tulibatizwa katika Kristo Yesu^h tulibatizwa katika kifo chake?ⁱ **4** Basi tulizikwa pamoja naye kupitia ubatizo wetu katika kifo chake,^j ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kupitia utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi pia tunapaswa tutembe katika hali mpya ya uzima.^k **5** Ikiwa tumeungana pamoja naye katika mfano wa kifo chake,^l hakika sisi pia tutaunganishwa pamoja naye katika mfano wa ufufuo wake.^m **6** Kwa maana tunajua kwamba utu wetu wa zamani ulitundikwa mtini pamoja naye,ⁿ ili mwili wetu wenye dhambi usiwe na nguvu,^o ili tusiendeleo kuwa watumwa wa dhambi.^p **7** Kwa maana yule ambaye amekufa ameondolewa* hatia ya dhambi yake.

6:7 *Au "amefunguliwa; amesamehewa."

SURA YA 5

a Ro 5:12

b Isa 53:11
Ebr 2:10c Ro 3:20
Gal 3:19

d 1Ko 15:56

e Yoh 3:16
1Yo 4:9

SURA YA 6

f 1Pe 2:24

g Ebr 10:26, 27

h 1Ko 12:13
Gal 3:27i Mk 10:38, 39
1Ko 15:29

j Kol 2:12

k Kol 3:10
1Yo 3:14l 2Ko 4:10
Flp 3:10

m 1Ko 15:42, 49

n Gal 5:24

o Kol 2:11
Kol 3:5

p 2Ko 7:1

Safu ya 2

a Mdo 13:34

b Ufu 1:17, 18

c Ebr 9:28
1Pe 3:18

d 1Pe 2:24

e Mwa 4:7

f Ro 12:1

g Ro 7:6
Gal 5:18
Kol 2:13, 14

h Yoh 1:17

i Ro 5:21

j 2Pe 2:19

k Yoh 8:34

l Ro 6:23

8 Isitoshe, ikiwa tumekufa pamoja na Kristo, tunaamini kwamba tutaishi pia pamoja naye. **9** Kwa maana tunajua kwamba Kristo, kwa kuwa sasa amefufuliwa kutoka kwa wafu,^a hatakuwa tena;^b kifo si bwana juu yake tena. **10** Kwa maana kifo alichokufa, alikuwa kuhusiana na dhambi* mara moja kwa wakati wote,^c lakini uhai anaishi, anaishi kuhusiana na Mungu. **11** Vivyo hivyo ninyi, mjihesabu kuwa wafu kuhusiana na dhambi lakini walio hai kuhusiana na Mungu kupitia Kristo Yesu.^d

12 Kwa hiyo, msiruhusu dhambi iendeleo kutawala kama mfalme katika miili yenu inayoweza kufa^e hivi kwamba msitii tamaa zake. **13** Wala msindelee kuitoa miili yenu* kwa dhambi kuwa silaha za ukosefu wa uadilifu, bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai kutoka kwa wafu, pia toeni miili yenu* kwa Mungu kuwa silaha za uadilifu.^f **14** Kwa maana dhambi haipaswi kuwa bwana juu yenu, kwa kuwa ninyi hamko chini ya sheria^g bali chini ya fadhili zisizostahiliwa.^h

15 Tuseme nini basi? Je, tufanye dhambi kwa sababu hatuko chini ya sheria bali chini ya fadhili zisizostahiliwa? La hash! **16** Je, hamjui kwamba mkijitoe kwa yeyote kuwa watumwa watiifu, ninyi ni watumwa wa yule mnayemtii,ⁱ ama watumwa wa dhambi^k inayotokeza kifo^l au wa utii unaotokeza uadilifu? **17** Lakini shukrani kwa Mungu kwamba ingawa wakati fulani mlikuwa watumwa wa

6:10 *Yaani, kuondoa dhambi. 6:13 *Tnn., "viungo vyenu."

dhambi, sasa mmekuwa watiifu kutoka moyoni kwa kielelezo cha fundisho mlilokabidhiwa. **18** Ndiyo, kwa kuwa mliwekwa huru kutoka katika dhambi,^a mmekuwa watumwa wa uadilifu.^b **19** Ninazungumza kwa maneno ya kibinadamu kwa sababu ya udhai-fu wa miili yenu; kwa maana kama mlivyovitoa viungo vyenu kuwa watumwa wa mambo machafu na uasi sheria unaotokeza uasi sheria, basi sasa vitoeni viungo vyenu viwe watumwa wa uadilifu unaotokeza utakatifu.^c **20** Kwa maana mlipokuwa watumwa wa dhambi, mlikuwa huru kuhusiana na uadilifu.

21 Basi, mlikuwa mkizaa matunda gani wakati huo? Mambo ambayo sasa mna-yaonea aibu. Kwa maana mwisho wa mambo hayo ni kifo.^d **22** Hata hivyo, sasa, kwa vile mliwekwa huru kutoka katika dhambi na kuwa watumwa wa Mungu, mnazaa matunda katika utakatifu,^e na mwisho ni uzima wa milele.^f **23** Kwa maana mshahara ambao dhambi hulipa ni kifo,^g lakini zawadi ambayo Mungu hutoa ni uzima wa milele^h kupitia Kristo Yesu Bwana yetu.ⁱ

7 Akina ndugu, je, inawezekana kwamba hamjui (kwa maana ninasema na wale wanaojua sheria) kuwa Sheria ni bwana juu wa mtu anapokuwa hai? **2** Kwa mfano, mwanamke aliyeo lewa amefungwa na sheria kwa mume wake akiwa hai; lakini mume wake akifa, yuko huru kutoka katika sheria ya mume wake.^j **3** Hivyo basi, mume wake akiwa hai, mwanamke huyo ataitwa mzinzi ikiwa atakuwa wa

SURA YA 6

a Yoh 8:31, 32

b 1Pe 2:24

c Ro 12:1

d Ro 8:6
Gal 5:19-21

e Gal 5:22, 23

f 1Ko 9:25

g Mwa 2:17

h Mt 25:46
1Pe 1:3, 4i 1Ti 1:16
1Yo 2:1, 2
Yud 21

SURA YA 7

j 1Ko 7:39

Safu ya 2

a Mt 5:32
Mt 19:9
Mk 10:11, 12
Lu 16:18b 1Ko 7:8, 9
1Ti 5:14

c 2Ko 11:2

d Mdo 5:30
2Ko 5:15e Gal 5:22, 23
Kol 1:10

f Yak 1:14, 15

g Ro 10:4
Efe 2:15
Kol 2:13, 14

h Ro 12:11

i Gal 3:10

j Ro 3:20
Gal 3:19k Kut 20:17
Kum 5:21l Ro 4:15
Ro 5:20

m 2Ko 3:6

n Law 18:5
Lu 10:26-28

mwanamume mwingine.^a Lakini mume wake akifa, yuko huru kutoka kwa sheria ya mume, basi mwanamke huyo si mzinzi ikiwa ataolewa na mwanamume mwingine.^b

4 Basi, ndugu zangu, ninyi pia mlifanywa wafu kuhusiana na Sheria kupitia mwili wa Kristo, ili muwe wa mwingine,^c yule aliyefufuliwa kutoka kwa wafu,^d ili tumzalie Mungu matunda.^e **5** Kwa maana tulipokuwa tukiishi kulingana na mwili, tamaa zenye dhambi zilizoamshwa na Sheria zilikuwa zikifanya kazi katika miili yetu* ili kuzaa matunda ya kifo.^f **6** Lakini sasa tumewekwa huru kutoka katika Sheria,^g kwa sababu tumekufa kwa kile ambacho kilituzua, ili tuwe watumwa katika maana mpya kwa roho,^h wala si katika maana ya zamani kwa sheria zilizoandikwa.ⁱ

7 Basi, tuseme nini? Je, Sheria ni dhambi? La hash! Kwa kweli, singejua dhambi ikiwa Sheria haingekuwapo.^j Kwa mfano, mimi singejua tamaa ikiwa Sheria haingesema: "Usitamani."^k **8** Lakini dhambi, kwa kutumia amri hiyo ilipata nafasi ya kutokeza ndani yangu tamaa ya kila aina, kwa maana bila sheria dhambi ilikuwa imekufa.^l **9** Kwa kweli, wakati mmoja nilikuwa hai bila sheria. Lakini amri ilipofika, dhambi ikawa hai tena, lakini mimi nikafa.^m **10** Na amri iliyokuwa ya kuongoza kwenye uzima,ⁿ niliona kuwa inaongoza kwenye kifo. **11** Kwa maana dhambi kwa kutumia amri hiyo ilipata nafasi ya kunishawishi na

7:5 *Tnn., "viungo vyetu."

kuniua kupitia amri. **12** Basi Sheria yenyewe ni takatifu, na amri ni takatifu na yenye uadilifu na ni njema.^a

13 Kwa hiyo, je, lililo jema lilinisababishia kifo? La ha-sha! Lakini dhambi ilifanya hivyo, ili ionyeshwe kuwa dhambi ndiyo inayoniletea kifo kupitia lile lililo jema,^b ili kupitia amri dhambi iwe mbaya zaidi.^c **14** Kwa maana tunajua kwamba Sheria ni ya kiroho, lakini mimi ni wa kimwili, nimeuzwa kwenye dhambi.^d

15 Kwa kuwa sielewi kile ninachokifanya. Kwa maana sifanyi kile ninachotaka, bali ninafanya kile ninachochukia.

16 Hata hivyo, ikiwa ninafanya jambo nisilotaka, nakubali kwamba Sheria ni nzuri.

17 Lakini sasa si mimi tena ninayelifanya, bali ni dhambi inayokaa ndani yangu.^e

18 Kwa maana najua kwamba ndani yangu, yaani, katika mwili wangu, halikai jambo lolote jema; kwa kuwa nina tamaa ya kufanya mambo mema lakini sina uwezo wa kuyafanya.^f

19 Kwa maana sifanyi jambo jema ninalotaka, bali ninafanya jambo baya nisilotaka.

20 Basi, ikiwa ninafanya jambo nisilotaka, si mimi tena ninayelifanya, bali ni dhambi inayokaa ndani yangu.

21 Basi, mimi naona sheria hii katika hali yangu: Ninapotaka kufanya yaliyo sawa, yaliyo mabaya yapo pamoja nami.^g

22 Kwa kweli naipenda sheria ya Mungu kulingana na mtu niliye kwa ndani,^h

23 lakini ninaona ndani ya mwili wangu* sheria nyingi-

7:23 *Tnn., "viungo vyangu."

SURA YA 7

a Kum 4:8
Zb 19:8

b 1Ko 15:56

c Ro 5:13

d Zb 5:15
Yoh 8:34
Ro 6:16

e Mwa 8:21

f Mt 26:41

g Yer 17:9

h 2Ko 4:16
Efe 3:16
Efe 4:23, 24

Safu ya 2

a Gal 5:17
Yak 4:1

b Yoh 8:34

c Ro 6:13
Gal 5:17

SURA YA 8

d Yoh 8:31, 32
Yak 1:25

e Ro 3:20
Ebr 7:11

f Ebr 7:18

g 1Yo 4:9

h Yoh 1:14

i Ro 3:31

j Gal 5:16, 18

k Gal 5:19-21

l Gal 5:22, 23

m Ro 6:21

n Gal 6:7, 8

o Isa 59:2
Kol 1:21

ne ikipigana na sheria ya akili yangu^a na kunichukua mateka kwa sheria ya dhambi^b iliyo ndani ya mwili wangu.*

24 Maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa kutoka katika mwili unaoapatwa na kifo hiki?

25 Shukrani kwa Mungu kupitia Yesu Kristo Bwana wetu! Basi, kwa akili yangu mimi ni mtumwa wa sheria ya Mungu, lakini kwa mwili wangu mimi ni mtumwa wa sheria ya dhambi.^c

8 Kwa hiyo, wale walio katika muungano na Kristo Yesu hawana hukumu ya hatia. **2** Kwa maana sheria ya roho ambayo hutokeza uzima katika muungano na Kristo Yesu imewaweka ninyi huru^d kutoka katika sheria ya dhambi na kifo. **3** Kile ambacho Sheria ilishindwa kufanya^e kwa sababu ilikuwa dhifu^f kupitia mwili, Mungu alifanya kwa kumtuma Mwana wake mwenyewe^g akiwa katika mfano wa mwili wenye dhambi^h na kuhusu dhambi, akiihukumu dhambi katika mwili,

4 ili takwa la uadilifu la Sheria litimizwe ndani yetuⁱ sisi tunaotembea, si kulingana na mwili, bali kulingana na roho.^j

5 Kwa kuwa wale wanaoishi kulingana na mwili hukaza akili zao kwenye mambo ya mwili,^k lakini wale wanaoishi kulingana na roho kwenye mambo ya roho.^l

6 Kwa maana kukaza akili kwenye mwili humaanisha kifo,^m lakini kukaza akili kwenye roho humaanisha uzima na amani;ⁿ

7 kwa sababu kukaza akili kwenye mwili humaanisha uadui na Mungu, kwa kuwa mwili haujitiishi kwa sheria ya Mungu,^o nao kwa kweli hauwe-

zi kujitiisha. **8** Basi wale wanaopatana na mwili hawawezi kumpendeza Mungu.

9 Hata hivyo, ninyi hampatani na mwili, bali mnapatana na roho,^a ikiwa kweli roho ya Mungu inakaa ndani yenu. Lakini ikiwa mtu yeyote hana roho ya Kristo, mtu huyo si wake. **10** Lakini ikiwa Kristo yuko katika muungano pamoja nanyi,^b mwili umekufa kwa sababu ya dhambi, bali roho ni uzima kwa sababu ya uadilifu. **11** Basi, ikiwa roho ya yule aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu inakaa ndani yenu, yule aliyemfufua Kristo Yesu kutoka kwa wafu^c ataifanya pia miili yenu inayoweza kufa iwe hai^d kupitia roho yake inayokaa ndani yenu.

12 Basi, akina ndugu, sisi tuna wajibu, si kwa mwili ili tuishi kulingana na mwili;^e **13** kwa maana ikiwa mnaishi kulingana na mwili hakika ninyi mtakufa; bali mkiyaua mazoea ya mwili^f kwa roho, mtaiishi.^g **14** Kwa maana wote wanaoongozwa na roho ya Mungu, kwa kweli ndio wana wa Mungu.^h **15** Kwa maana hamkupokea roho ya utumwa inayosababisha woga tena, bali mlipokea roho ya kufanywa kuwa wana, roho ambayo kupitia hiyo tunapaza sauti: “Abba,* Baba!”ⁱ **16** Roho yenyewe hutoa ushahidi pamoja na roho yetu/ kwamba sisi ni watoto wa Mungu.^k **17** Basi, ikiwa sisi ni watoto, sisi pia ni warithi—warithi wa Mungu kwelikweli, lakini warithi pamoja/ na Kristo—mradi tu tunateseka pamoja^m ili pia tutukuzwe pamoja.ⁿ

8:15 *Neno la Kiebrania au Kiaramu linalomaanisha “Ee Baba!”

SURA YA 8

a Gal 5:25

b Yoh 15:4

c Mdo 2:24

d Efe 2:1, 5

e Gal 5:19-21

f 1Ko 9:27
Gal 5:24
Efe 4:22
Kol 3:5

g Gal 6:7, 8

h Yoh 1:12
Yoh 3:5

i Gal 4:4-6

j 1Ko 2:10, 12
2Ko 1:22k Yoh 1:12
Gal 3:26
1Yo 3:2l Lu 12:32
Gal 3:29m Flp 1:29
Kol 1:24n 1Ko 15:53
Ufu 3:21

Safu ya 2

a 2Ko 4:17
1Pe 4:13

b 1Yo 3:2

c Mwa 3:17-19

d Yoh 8:31, 32
1Ko 15:22

e 2Ko 5:1, 2

f Gal 4:4, 5
Efe 1:5
Ufu 21:7

g 1Pe 1:3, 4

h 2Ko 5:7

i Ro 5:3-5

j Yoh 14:16, 26
Yoh 16:7

k Yer 11:20

18 Kwa maana ninaona kwamba mateso ya wakati huu si kitu yakilinganishwa na utukufu utakaofunuliwa ndani yetu.^a **19** Kwa kuwa uumbaji unangojea na kutazamia kwa hamu kufunuliwa kwa wana wa Mungu.^b **20** Kwa maana uumbaji ulitiishwa chini ya ubatili,^c si kwa mapenzi yake wenyewe bali kupitia yule aliyetiisha, kwa msingi wa tumaini **21** kwamba uumbaji wenyewe pia utawekwa huru^d kutoka katika utumwa wa uharibifu na kuwa na uhuru wenye utukufu wa watoto wa Mungu. **22** Kwa maana tunajua kwamba uumbaji wote unaendelea kuugua pamoja na kuwa katika maumivu pamoja mpaka sasa. **23** Si hilo tu, bali sisi wenyewe pia tulio na matunda ya kwanza, yaani, ile roho, ndiyo, sisi wenyewe tunaugua ndani yetu wenyewe,^e huku tuingojea kwa hamu kufanywa kuwa wana,^f kuachiliwa huru kutoka kwenye miili yetu kupitia fidia. **24** Kwa maana tuliokolewa katika tumaini hili; lakini tumaini linaloonekana si tumaini, kwa kuwa mtu anapoona kitu, je, yeye hukitumainia? **25** Lakini tukitumainia^g kile ambacho hatuoni,^h sisi huendelea kukisubiri kwa hamu na uvumilivu.ⁱ

26 Vivyo hivyo, roho pia hutoa msaada kwa ajili ya udhai-fu wetu;^j kwa maana tatizo ni kwamba hatujui kile tunachopaswa kusali kuhusu kama tunavyohitaji, lakini roho yenyewe hutuombea kwa kuugua kusikotamkwa.* **27** Lakini yule anayechunguza mioyo^k

8:26 *Au “kusikosemwa.”

anajua maana ya roho, kwa sababu inaomba kupatana na Mungu kwa ajili ya watakatifu.

28 Tunajua kwamba Mungu huzifanya kazi zake zote zishirikiane pamoja kwa ajili ya mema ya wale wanaompenda Mungu, wale ambao wameitwa kulingana na kusu-di lake;^a **29** kwa sababu wale aliowatambua kwanza, aliwachagua awali pia wafananishwe na mfano wa Mwana wake,^b ili awe mzaliwa wa kwanza^c kati ya ndugu wengi.^d **30** Isitoshe, wale aliowachagua awali^e ndio aliowaita pia;^f na wale aliowaita ndio aliowatangaza kuwa waadilifu pia.^g Mwishowe wale aliowatanga za kuwa waadilifu ndio aliowatukuza pia.^h

31 Basi, tuseme nini kuhusu mambo haya? Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani atakayekuwa dhidi yetu?ⁱ **32** Kwa kuwa hakusita kumtoa hata Mwana wake mwenyewe bali alimkabidhi kwa ajili yetu sote,^j je, hatatupa pia pamoja naye kwa fadhili vitu vingine vyote? **33** Ni nani atakayewashtaki waliochaguliwa wa Mungu?^k Mungu Ndiye anayewatanga kuwa waadilifu.^l **34** Ni nani atakayewahukumu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa, ndiyo, isitoshe, yeye ndiye aliyefufuliwa, aliye kwenye mkono wa kuumbe wa Mungu^m na ambaye pia hutuombea.ⁿ

35 Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo?^o Je, ni dhiki au taabu au mate-so au njaa au uchi au hataru au upanga?^p **36** Kama ilivyoandikwa: "Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa; tu-

SURA YA 8

a Efe 1:9-11
2Ti 1:9

b Yoh 13:15
Ro 6:5
1Ko 15:49

c Ebr 1:6

d Ebr 2:11

e Efe 1:5

f Flp 3:14
1Th 2:12
Ebr 3:1

g Ro 5:18
Tit 3:7

h 2Ko 4:6

i Zb 118:6
1Yo 4:4

j Yoh 3:16
Ro 3:25
1Yo 4:9

k Isa 50:8

l Mdo 13:38, 39
Ebr 10:16, 17

m Zb 110:1

n Ebr 7:25
1Yo 2:1

o Yoh 15:10

p 2Ko 4:8, 9

Safu ya 2

a Zb 44:22

b Yoh 16:33

c Efe 6:12

SURA YA 9

d Kut 4:22

e Mdo 3:25
Mdo 7:8

f Kut 24:12

g Mdo 26:7
Ebr 9:1

h Ro 4:13

i Kum 10:15

j Mt 1:17

k Ro 2:28
Ufu 2:9

l Yoh 8:39
Gal 3:29

m Mwa 21:12
Ebr 11:18

mehesabiwa kuwa kondoo wa kuchinjwa."^a **37** Badala yake, katika mambo haya yote tunatoka tukiwa tumeshinda kabisa^b kupitia yule aliyetupenda. **38** Kwa maana nime-sadiki kwamba wala kifo wala uzima wala malaika wala serikali wala mambo yaliyopo sasa wala mambo yatakayokuja wala nguvu^c **39** wala kimo wala kina wala uumbaji mwingine wowote havitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.

9 Ninasema kweli katika Kristo; sisemi uwongo, kama dhamiri yangu inavyonitolea ushahidi katika roho takatifu, **2** kwamba nina huzuni kubwa na maumivu yasiyoi-sha moyoni mwangu. **3** Kwa maana ningetamani mimi mwenyewe nitenganishwe na Kristo, niwe aliyelaaniwa kwa ajili ya ndugu zangu, watu wangu wa ukoo kulingana na mwili, **4** ambao ni Waisraeli. Wao ndio waliofanywa kuwa wana^d na kupewa utukufu na maagano^e na Sheria^f na utumishi mtakatifu^g na ahadi.^h **5** Wao ni uzao wa mababu,ⁱ na Kristo alitoka kwao kulingana na mwili.^j Mungu, aliye juu ya wote, asifiwe milele. Amina.

6 Hata hivyo, si kwamba neno la Mungu limeshindwa. Kwa maana si wote wanaotokana na Israeli ni "Israeli" kihalisi.^k **7** Wala si wote walio watoto kwa sababu wao ni uzao wa* Abrahamu;^l badala yake, "Ule utakaoitwa uzao wako[#] utapitia kwa Isaka."^m

8 Yaani, watoto katika mwili
9:7 *Tnn., "mbegu ya." #Tnn., "mbegu yako."

li si watoto wa Mungu kihali-si,^a lakini watoto kupitia ahadi^b ndio wanaohesabiwa kuwa uzao.* **9** Kwa maana neno la ahadi lilisema hivi: “Nitakuja wakati huu, na Sara atakuwa na mwana.”^c **10** Lakini si wakati huo tu, bali pia Rebeka alipopata mimba ya mapacha kupitia yule mwanamume mmoja, Isaka babu yetu;^d **11** kwa maana walipokuwa bado hawajazaliwa wala kufanya jambo lolote jema au baya, ili kusudi la Mungu kuhusu kuchagua liendelee kutegemea, si matendo, bali Yule ambaye huita, **12** Rebeka aliambiwa: “Mkubwa atakuwa mtumwa wa mdogo.”^e **13** Kama ilivyoandikwa: “Nilimpenda Yakobo, lakini nikamchukia Esau.”^f

14 Basi, tuseme nini? Je, Mungu ana ukosefu wa haki? La hashah!^g **15** Kwa maana anamwambia Musa: “Nitamwonyesha rehema yeyote ninayetaka kumwonyesha rehema, nami nitamhurumia yeyote ninayetaka kumhurumia.”^h **16** Hivyo basi, haitegemei jinsi mtu anavyotamani au jitihada zake,* bali inategemea Mungu, aliye na rehema.ⁱ **17** Kwa maana andiko lina-mwambia Farao: “Kwa sababu hii nimekuacha ubaki: ili nionyeshe nguvu zangu kuhusiana na wewe na ili jina langu litangazwe katika dunia yote.”^j **18** Hivyo basi, yeye humwonyesha rehema yeyote anayetaka, lakini yeye humwacha yeyote anayetaka awe mkaidi.^k

19 Kwa hiyo utaniiliza: “Kwa nini bado analaumu? Kwa maana ni nani amba-

9:8 *Tnn., “mbegu.” 9:16 *Tnn., “yule anayetaka wala yule anayekimbia.”

SURA YA 9

a Yoh 1:12,13

b Gal 4:28

c Mwa 18:10,14

d Mwa 25:21,24

e Mwa 25:23

f Mal 1:2,3
Ebr 12:16g Kum 32:4
Ayu 34:10

h Kut 33:19

i Tit 3:4,5

j Kut 9:16

k Kut 10:1
Kut 14:4

Safu ya 2

a Ayu 40:2

b Isa 29:16
Isa 45:9c Isa 64:8
Yer 18:6

d 1Th 5:9

e Ro 11:13
Efe 3:6

f Efe 2:12

g Ho 2:23
Mt 21:43
1Pe 2:10h Ho 1:10
Gal 3:26i Ho 1:10
Ro 11:4,5

ye amepinga mapenzi yake?”

20 Lakini ewe mwanadamu wewe ni nani hata uthubutu kumjibu Mungu?^a Je, kitu kilichofinyangwa kitamwambia yule aliyekifinyanga: “Kwa nini ulinitengeneza hivi?”^b

21 Kwani, je, mfinyanzi hana mamlaka juu ya udongo^c kufanya kutokana na donge lililele chombo kimoja kwa matumizi yenye kuheshimika, na kingine kwa matumizi yasiyo ya kuheshimika? **22** Inakuwaje basi, ikiwa Mungu, ingawa alikuwa na nia ya kuonyesha ghadhabu yake na kujulisha nguvu zake, alivumilia kwa subira nyingi vyombo vya ghadhabu vilivyo tayari kwa ajili ya uharibifu? **23** Na ikiwa hilo lilifanywa ili ajulishwe utajiri wa utukufu wake kwa vyombo vya rehema,^d alivyotayarisha awali kwa ajili ya utukufu, **24** yaani, sisi, ambao alituita si kutoka kati ya Wayahudi peke yao bali pia kutoka kati ya mataifa,^e kuna ubaya gani? **25** Ni kama anvyosema pia katika Hosea: “Wale ambao si watu wangu^f nitawaita ‘watu wangu,’ na mwanamke ambaye hakupe-ndwa, nitamwita ‘mpendwa’;^g **26** na mahali ambapo waliambiwa, ‘Ninyi si watu wangu,’ hapo wataitwa ‘wana wa Mungu aliye hai.’”^h

27 Isitoshe, Isaya anapaza sauti kuhusu Israeli: “Ijapokuwa idadi ya wana wa Israeli huenda ikawa kama chembe za mchanga wa bahari, ni watu wachache tu waliobaki watakaokolewa.ⁱ **28** Kwa maana Yehova* atatoza hesabu duniani, na kuimaliza na

9:28 *Angalia Nyongeza A5.

kuifupisha.”^a **29** Pia, kama Isaya alivyotabiri: “Kama Yehova* wa majeshi hangetuachia uzao,[#] tungekuwa kama Sodoma, na tungefanana na Gomora.”^b

30 Basi, tuseme nini? Kwa mba watu wa mataifa, ingawa hawakuwa wakiufuatilia uadilifu,^c waliufikia uadilifu, uadilifu unaotokana na imani;^d **31** lakini Israeli, ingawa walikuwa wakiufuatilia sheria ya uadilifu, hawakuifikia sheria. **32** Kwa sababu gani? Kwa sababu waliufuatilia, si kwa imani, bali kama kwa matendo. Walijikwa kwenye “jiwe la kukwaza”;^e **33** kama ilivyoandikwa: “Tazama! Ninaweka katika Sayuni jiwe^f la kukwaza na mwamba wa kuangusha, lakini yeye anayemwamini hatakata tamaa.”^g

10 Akina ndugu, nia njema ya moyo wangu na dua yangu kwa Mungu kwa ajili yao, kwa kweli, ni kwa ajili ya wokovu wao.^h **2** Kwa maana ninawatolea ushahidi kwamba wana bidii kwa ajili ya Mungu,ⁱ lakini si kulingana na ujuzi sahihi. **3** Kwa sababu ya kutojua uadilifu wa Mungu/ bali wakijaribu kujiwekea uadilifu wao wenyewe,^k hawakujitiisha kwa uadilifu wa Mungu.^l **4** Kwa maana Kristo ndiye mwisho wa Sheria,^m ili kila mtu aliye na imani* awe na uadilifu.ⁿ

5 Kwa kuwa Musa anaandika hivi kuhusu uadilifu kupitia Sheria: “Mtu anayefanya mambo hayo ataishi kupitia

9:28 *Au “kuifanya haraka.” 9:29; 10:13 *Angalia Nyongeza A5. 9:29 #Tnn., “mbegu.” 10:4 *Au “anayeonyesha imani.”

SURA YA 9

a Isa 10:22, 23

b Isa 1:9

c Ro 10:20

d Ro 4:11

Flp 3:9

e Isa 8:14
Lu 20:17, 18
1Ko 1:23f Zb 118:22
Mt 21:42g Isa 28:16
Ro 10:11
1Pe 2:6

SURA YA 10

h Ro 9:3, 4

i Mdo 21:20
Gal 1:14

j Ro 1:16, 17

k Lu 16:15
Flp 3:9

l Lu 7:29, 30

m Mt 5:17
Ro 7:6
Efe 2:15
Kol 2:13, 14

n Gal 3:24

Safu ya 2

a Law 18:5
Gal 3:12

b Kum 9:4

c Kum 30:12

d Kum 30:13

e Kum 30:14

f Mdo 16:31

g 1Ko 9:16
2Ko 4:13
Ebr 13:15h Isa 28:16
Ro 9:33i Mdo 15:7-9
Gal 3:28j Yoe 2:32
Mdo 2:21

k Mt 28:19, 20

l Isa 52:7
Efe 6:14, 15

mambo hayo.”^a **6** Lakini uadilifu unaotokana na imani husema: “Usiseme moyoni mwako,^b ‘Ni nani atakayepanda juu mbinguni?’^c yaani, kumleta Kristo chini, **7** au, ‘Ni nani atakayeshuka katika shimo?’^d yaani, kumleta Kristo juu kutoka kwa wafu.” **8** Lakini linasema nini? “Neno hilo liko karibu nawe, katika kinywa chako na katika moyo wako mwenyewe”;^e yaani, “neno” la imani, ambalo sisi tunahubiri. **9** Kwa maana ukitangaza waziwazi kwa kinywa chako kwamba Yesu ni Bwana,^f na kuwa na imani moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokolewa. **10** Kwa sababu kwa moyo mtu huwa na imani ili apate uadilifu, lakini kwa kinywa mtu hufanya tangaizo la hadharani^g ili apate wokovu.

11 Kwa kuwa andiko lina-sema: “Yeyote anayemwamini hatakata tamaa.”^h **12** Kwa maana hakuna tofauti kati ya Myahudi na Mgiriki.ⁱ Kuna Bwana yuleyule juu ya wote, aliye tajiri* kwa wote wanaomwitia. **13** Kwa maana “kila mtu anayeliitia jina la Yehova* ataokolewa.”^j **14** Hata hivyo, watawezaje kumwitia ikiwa hawajamwamini? Nao watawaminije yule ambaye hawajamsikia? Nao watasikia-je bila mtu wa kuhubiri? **15** Nao watahubirije isipokuwa wawe wametumwa?^k Kama ilivyoandikwa: “Jinsi inavyopendeza miguu ya wale wanaotangaza habari njema ya mambo mema!”^l

10:7 *Au “abiso.” Angalia Kamusi, uku. 2012. 10:12 *Au “mkarimu.”

16 Hata hivyo, si wote waliotii habari njema. Kwa maana Isaya anasema: "Yehova,* ni nani ambaye ameamini jambo alilosikia kutoka kwe-tu?"^{#a} **17** Kwa hiyo imani hu-fuata jambo lililosikiwa.^b Nalo jambo lililosikiwa ni kupitia neno kumhusu Kristo. **18** Lakini ninauliza, je, walikosa kusikia? Kwa kweli, "sau-ti yao ilifika katika dunia yote, na ujumbe wao ulifika mpaka kwenye miisho ya dunia inayokaliwa."^c **19** Lakini ninauliza, je, kweli Israeli walikosa kujua?^d Kwanza Musa anasema: "Nitawachochea muwe na wivu kupitia lile ambalo si taifa; nitawachochea muwe na hasira kali kupitia taifa lenye ujinga."^e **20** Lakini Isaya anakuwa na ujasiri sana na kusema: "Wale ambao hawakuwa wakinitafuta walini-pata;^f wale ambao hawakuwa wakiuliza juu yangu walini-jua."^g **21** Lakini anasema kuhusiana na Israeli: "Mchana kutwa nimewanyooshea miko-no yangu watu wasiotii na wakaidi."^h

11 Basi ninauliza, je, Mungu aliwakataa watu wake?ⁱ La hashah! Kwa maana mimi pia ni Mwisraeli, wa uzao wa* Abrahamu, kutoka kabila la Benjamini. **2** Mungu hakuwakataa watu wake, aliwatambua kwanza.^j Je, hamjui andiko linavyosema kumhusu Eliya, anapomsihi Mungu dhidi ya Israeli? **3** "Yehova,* wamewaua manabii wako, wamezibomoa madhabahu zako, nami peke yangu nimebaki,

10:16; 11:3 *Angalia Nyongeza A5. 10:16 #Au "ujumbe wetu." 11:1 *Tnn., "mbegu ya."

SURA YA 10

a Isa 53:1
Yoh 12:37, 38

b Yoh 4:42

c Zb 19:4
Mdo 1:8

d Mt 10:5, 6
Mdo 2:14

e Kum 32:21

f Ro 9:30

g Isa 65:1

h Isa 65:2

SURA YA 11

i Isa 12:22
Yer 31:37

j Kut 19:5
Zb 94:14

Safu ya 2

a 1Fa 19:2, 14

b 1Fa 19:18

c Ro 9:27

d Efe 1:7
Efe 2:8

e Gal 2:15, 16

f Yoh 1:11, 12

g 2Ko 3:14, 15

h Isa 29:10

i Kum 29:4

j Zb 69:22, 23

k Kum 32:21
Ro 10:19

l Ro 9:23, 24

na sasa wanajaribu kuniua."^{*a} **4** Lakini neno la Mungu linamwambia nini? "Nimeacha watu 7,000 kwa ajili yangu, watu ambao hawakumpigia goti Baali."^b **5** Basi, kwa njia hiyohiyo, wakati huu pia, kuna mabaki kulingana na kuchaguliwa^c kupitia fadhili zisizostahiliwa. **6** Basi ikiwa ni kupitia fadhili zisizostahiliwa,^d si kupitia matendo tena;^e la sivyo, fadhili zisizostahiliwa hazingekuwa tena fadhili zisizostahiliwa.

7 Tuseme nini, basi? Jambo lililele ambalo Israeli anatafuta kwa bidii hakulipata, lakini wale waliochaguliwa walilipata.^f Hisia za wale wengine zilifanywa kuwa nzito,^g **8** kama ilivyoandikwa: "Mungu amewapa roho ya usingizi mzito,^h macho yasiyoona na masikio yasiyosikia, mpaka leo hii."ⁱ **9** Pia, Daudi anasema: "Meza yao na iwe kitu kinachonasa na mtego na kikwazo na malipo kwao. **10** Acha macho yao yatiwe giza wasiweze kuona, na sikuzote uwafanye wainamishe migongo yao."^j

11 Basi ninauliza, Je, walijikwaa na kuanguka kabisa? La hashah! Lakini kwa kujikwaa kwao, kuna wokuvu kwa watu wa mataifa, ili kuwachochea wawe na wivu.^k **12** Sasa ikiwa kujikwaa kwao humaanisha utajiri kwa ulimwengu, na kupungua kwao humaanisha utajiri kwa watu wa mataifa,^l je, idadi yao kamili haitamaanisha hivyo hata zaidi?

13 Sasa ninazungumza nani mlio watu wa mataifa. Kwa

11:3 *Au "kuchukua uhai (nafsi) wangu."

kuwa mimi ni mtume kwa mataifa,^a ninaitukuza* huduma yangu,^b **14** ili kuona ikiwa ninaweza kwa njia fulani kuwachochea watu wangu wawe* na wivu na kuwaokoa baadhi yao. **15** Kwa maana ikiwa kutupwa kwao^c humaanisha upatanisho kwa ulimwengu, kukubaliwa kwao kutamaanisha nini isipokuwa uzima kutoka kwa wafu? **16** Isitoshe, ikiwa sehemu ya donge inayochukuliwa iwe matunda ya kwanza ni takatifu, donge lote pia ni takatifu; na ikiwa mzizi ni mtakatifu, matawi pia yako hivyo.

17 Hata hivyo, ikiwa baadhi ya matawi yalikatwa, na ingawa wewe ni mzeituni wa mwituni, ulipandikizwa kati yake na kuwa mshiriki wa utajiri wa mzizi wa mzeituni, **18** usijivune* dhidi ya matawi. Kama ukijivuna[#] dhidi yake,^d kumbuka kwamba, si wewe unayebeba mzizi, bali mzizi unakubeba wewe. **19** Basi, utasema: "Matawi yalikatwa ili mimi nipandikizwe."^e **20** Hilo ni kweli! Walikatwa^f kwa sababu walikosa imani, lakini wewe umesimama kwa imani.^g Usiwe na majivuno, bali uwe na woga. **21** Kwa maana ikiwa Mungu hakuyaacha matawi ya asili, vivyo hivyo hatakuacha wewe. **22** Kwa hiyo, fikiria fadhili^h na ukali wa Mungu. Kuna ukali kuwaelekea wale walioanguka,ⁱ lakini kukuelekea wewe kuna fadhili za Mungu mradi tu ukae katika fadhili zake; la sivyo, wewe pia utakatwa. **23** Wao pia, ikiwa

11:13 *Au "ninaisifu." 11:14 *Tnn., "mwili wangu uwe." 11:18 *Au "usijigamba." # Au "ukijigamba."

SURA YA 11

a Mdo 9:15
Gal 1:15, 16
Efe 3:8

b Mdo 28:30, 31
Kol 1:23
2Ti 4:5

c Mt 21:43

d 1Ko 10:12

e Mdo 15:14

f Mt 21:43

g Efe 2:8

h Ro 2:4

i Mt 23:38

Safu ya 2

a Mdo 2:38

b Efe 3:5, 6

c Ro 2:29
Ro 9:6
Gal 3:29

d Zb 14:7

e Isa 59:20, 21

f Isa 27:9

g Kum 10:15

h Efe 2:1, 2

i Mdo 15:7-9

j Mdo 7:51

k Ro 3:9

l 1Ti 2:3, 4

hawataendelea kukosa imani, watapandikizwa,^a kwa kuwa Mungu anaweza kuwapandikiza tena. **24** Kwa maana ikiwa wewe ulikatwa kutoka kwenye mzeituni wa mwituni na kupandikizwa kinyume cha asili kwenye mzeituni wa bustani, je, hawa walio wa asili hawatapandikizwa tena kwenye mzeituni wao wenyewe?

25 Kwa maana sitaki ninyi, akina ndugu, mkose kujua siri hii takatifu,^b ili msiwe wenyewe hekima machoni penu wenyewe: Hisia za Israeli zimetiwa uzito kwa kiasi fulani mpaika idadi kamili ya watu wa mataifa itakapoingia, **26** na kwa njia hii Israeli wote^c wataokolewa. Kama ilivyoandikwa: "Mkombozi* atakuja kutoka Sayuni^d na kuondoa mazoea ya kutomwogopa Mungu kutoka katika Yakobo. **27** Na hili ndilo agano langu pamoja nao,^e nitakapoondoa dhambi zao."^f **28** Ni kweli, kuhusu habari njema wao ni adui kwa ajili yenu, lakini kuhusu uchaguzi wa Mungu wao ni wapendwa kwa ajili ya mababu zao.^g **29** Kwa kuwa Mungu hataghairi kwa sababu ya zawadi na mwito anaotoa. **30** Kwa maana kama vile ninyi wakati fulani mlivyokuwa watu wasiomtii Mungu^h lakini sasa mmeonyeshwa rehemaⁱ kwa sababu ya kutotii kwao,^j **31** ndivyo pia hawa sasa wamekuwa wasiotii na hivyo mkaonyeshwa rehema, ili wao wenyewe pia waonyeshwe rehema sasa. **32** Kwa maana Mungu amewaweka wote pamoja katika kutotii,^k ili awaonyeshe wote rehema.^l

11:26 *Au "Mwokozi."

33 Lo! Jinsi kilivyo kina cha utajiri wa Mungu na hekima na ujuzi! Jinsi hukumu zake zisivyochunguzika na njia zake zisivyotafutika! **34** Kwa maana “ni nani amejua akili ya Yehova,* au ni nani amekuwa mshauri wake?”^a **35** Au, “Ni nani amempa yeye kwanza, hivi kwamba iwe lazima arudishiwe?”^b **36** Kwa sababu vitu vyote vimetoka kwake, kupitia yeye na kwa ajili yake. Kwake yeye na kuwe na utukufu milele. Amina.

12 Kwa hiyo akina ndugu, ninawasihi kwa huruma za Mungu, mtoe miili yenu^c iwe dhahibu iliyo hai, takatifu,^d na yenye kukubalika kwa Mungu, utumishi mtakatifu pamoja na nguvu zenu za kufikiri.^e **2** Na acheni kufinyangwa na mfumo huu wa mambo,* bali mgeuzwe kwa kufanya upya akili yenu,^f ili mjihakikishie wenyewe^g mapenzi ya Mungu yaliyo mema na yenye kukubalika na makamilifu.

3 Kwa maana kupitia fadhili zisizostahiliwa nilizopewa ninamwambia kila mtu kati yenu asijifikirie mwenyewe kuliko ilivyo lazima kufikiri,^h bali afikiri ili awe na akili timamu, kila mmoja kama Mungu alivyompa* kipimo cha imani.ⁱ **4** Kwa maana kama vile tulivyo na viungo vingi katika mwili mmoja,^j lakini viungo hivyo havifanyi kazi ileile, **5** ndivyo sisi, ingawa tuko wengi, ni mwili mmoja katika muungano na Kristo, lakini kila mmoja wetu ni kiu-

11:34; 12:11 *Angalia Nyongeza A5. **12:2** *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mfumo wa mambo.” **12:3** *Au “alivyomgawia.”

SURA YA 11

a Isa 40:13

Da 4:35

b Ayu 41:11

SURA YA 12

c Ro 6:13

d 2Ko 7:1

1Pe 1:15

e 2Ti 1:7

f Efe 4:23, 24

g 1Ti 4:15

h Met 16:18

Gal 6:3

1Pe 5:5

i Efe 2:8

j 1Ko 12:12

Safu ya 2

a 1Ko 12:25

b Efe 3:7

c 1Ti 5:17

1Pe 4:10, 11

d 2Ti 4:2

e Kum 15:11

2Ko 8:2

f 1Th 5:12

1Pe 5:2

g Efe 4:32

h 1Ti 1:5

Yak 3:17

1Pe 1:22

i Zb 97:10

Met 8:13

j Flp 2:3

k Met 13:4

l Mdo 18:24, 25

m Ro 6:22

n Mdo 14:22

o Flp 4:6

1Th 5:17

p Met 3:27

1Yo 3:17

q 1Pe 4:9

3Yo 8

r Mt 5:44

Lu 6:27, 28

s Yak 3:9, 10

ngo cha mwingine.^a **6** Basi, kwa kuwa tuna zawadi zinzotofautiana kulingana na fadhili zisizostahiliwa tulizopewa,^b kama ni ya unabii, na tuteo unabii kulingana na imani yetu; **7** au kama ni ya huduma, na tuwe katika huduma hii; au yule anayefundisha, na aendelee kufundisha;^c **8** au yule anayeta moyo,* na atie moyo;^d yule anayegawa,^e na afanye hivyo kwa ukarimu;^e yule anayesimamia,^g na afanye hivyo kwa bidii;^f yule anayeonyesha rehema, na afanye hivyo kwa uchangamfu.^g

9 Upendo wenu na uwe bila unafiki.^h Chukieni mauvu;ⁱ shikamaneni na mema. **10** Katika upendo wa kindugu iweni na upendo mworo kwa mtu na mwenzake. Katika kuonyeshana heshima, iweni wa kwanza.*^j **11** Iweni wenye bidii,^k msiwe waviyu.^{ak} Wakeni roho.^l Mtumikieni Yehova.*^m **12** Shangilieni katika tumaini. Vumilieni chini ya dhiki.ⁿ Dumuni katika sala.^o **13** Shirikini pamoja na watakatifu kulingana na mahitaji yao.^p Iweni wakaribishaji wageni.*^q **14** Endeeleni kuwabariki wale wanaowatesa;^r muwe mkibariki msiwe mkilaani.^s **15** Shangilieni na wale wanaoshangilia; lieni na wale wanaolia. **16** Wafiki-rieni wengine kama mnavyojifikiria; msikazie akili zenu kwenye mambo makuu,* bali

12:8 *Au “anayehimiza.” ^aAu “ahimiza.” ^bAu “anayechangia.” ^cAu “anayeongoza.” ^dAu “juhudi.” **12:10** *Au “chukueni hatua ya kwanza.” **12:11** *Au “jitihada.” ^eAu “msiwe waviyu katika kazi zenu.” **12:13** *Au “iweni wakarimu.” **12:16** *Au “msifikirie makuu.”

mwongozwe na mambo ya hali ya chini.^a Msiwe wenye heki-ma machoni penu wenyewe.^b

17 Msimilipe yeyote uovu kwa uovu.^c Zingatieni mambo yaliyo mema kulingana na maoni ya* watu wote. **18** Ikiwezekana, kwa kadiri inavyo-wategemea ninyi, fanyeni amani na watu wote.^d **19** Wapendwa, msijilipizie kisasi bali iachieni nafasi ghadhabu,*^e kwa maana imeandikwa: "Kisasi ni changu; mimi nitalipa, asema Yehova."^f **20** Lakini, "ikiwa adui yako ana njaa, mli-she; ikiwa ana kiu, mpe kitu anywe; kwa maana kwa kufanya hivyo utakusanya ma-kaa ya mawe yanayowaka juu ya kichwa chake."^g **21** Usia-che ushindwe na uovu, bali endelea kuushinda uovu kwa wema.^h

13 Kila mtu na ajitiishe* kwa mamlaka zilizo ku-bwa,ⁱ kwa maana hakuna mamlaka isipokuwa kupitia Mungu;^j mamlaka zilizo-pi zimewekwa na Mungu katika vyeo vyao vya kadiri.^k **2** Kwa hiyo, yeyote anayepinga mam-laka amechukua msimamo dhidi ya mpango wa Mungu; wale ambao wamechukua msimamo dhidi ya mpango huo, watajiletea hukumu wao we-nyewe. **3** Kwa maana wata-wala ni kitu cha kuogopesha, si kwa tendo jema, bali kwa baya.^l Je, unataka usiogope hiyo mamlaka? Endelea kufa-nya mema,^m nayo itakusifu; **4** kwa maana hiyo ni mhudu-mu wa Mungu kwako kwa fai-

12:17 *Au "machoni pa." 12:19 *Yaani, ghadhabu ya Mungu. #Angalia Nyo-ungeza A5. 12:20 *Yaani, kupunguza uadui wake na kuyeyusha ugumu wake. 13:1 *Au "Kila nafsi na ijitiishe."

SURA YA 12

a Lu 14:10
Lu 22:24-26
Yoh 13:14
Flp 2:3

b Ayu 37:24
Met 3:7

c 1Th 5:15
1Pe 2:23
1Pe 3:9

d 2Ti 2:24
Ebr 12:14
Yak 3:18

e Law 19:18
Mt 5:39

f Kum 32:35
Ebr 10:30

g Met 25:21, 22

h Kut 23:4
Mt 5:44
Lu 6:27

SURA YA 13

i Tit 3:1
1Pe 2:13, 14

j Yoh 19:10, 11

k Mdo 17:26

l 1Pe 2:13, 14

m 1Pe 3:13

Safu ya 2

a 1Pe 2:19
1Pe 3:16

b Mt 22:21
Mk 12:17
Lu 20:25

c Met 24:21

d 1Pe 2:13, 17

e Kol 3:14
1Ti 1:5
1Yo 4:11

f Gal 5:14
Yak 2:8

g Kut 20:14
Mt 5:27, 28
1Ko 6:9, 10

h Mwa 9:6
Kum 5:17

i Kut 20:15

j Kut 20:17

k Law 19:18
Mt 22:39

l Lu 6:31
2Ti 2:24

m Mt 22:37-40

n Lu 21:36
1Th 5:6

o Efe 5:10, 11

da yako. Lakini ikiwa unafanya mabaya, ogopa, kwa maana haichukui upanga bila kusudi. Hiyo ni mhudumu wa Mungu, nayo hulipiza kisasi ili kuonyesha ghadhabu* dhidi ya yule anayefanya mabaya.

5 Kwa hiyo kuna sababu ya lazima kwenu kujitiisisha, si kwa sababu ya ghadhabu hiyo tu, bali pia kwa sababu ya dhamiri yenu.^a **6** Ndiyo maana mnalipa kodi pia; kwa kuwa wao ni watumishi wa Mungu kwa watu wote wakitumikia daima kwa kusudi hili. **7** Wapeni wote haki zao: yule anayetaka kodi, kodi;^b yule anayetaka ushuru, ushuru; yule anayetaka woga, woga huo;^c yule anayetaka heshima, heshima hiyo.^d

8 Msiwe na deni lolote kwa mtu yeyote, isipokuwa kupendana,^e kwa maana yeyote anayempenda mwanadamu mwenzake ameitimiza sheria.^f **9** Kwa maana sheria zinazosema, "Usifanye uzinzi,^g usiue,^h usiibe,ⁱ usitamani,"^j na amri nyingine yoyote iliyo-po, zimejumlishwa katika maneno haya: "Lazima umpende jirani yako kama unavyoji-penda mwenyewe."^k **10** Upendo haumfanyii uovu jirani;^l kwa hiyo, upendo ndio utimizo wa sheria.^m

11 Nanyi fanyeni hivi kwa sababu mnayajua majira, kwamba tayari ni saa yenu ya kuamka kutoka usingizini,ⁿ kwa maana sasa wokovu wetu uko karibu zaidi kuliko wakati tulipoanza kuamini. **12** Usiku umesonga sana; mchana umekaribia. Kwa hiyo, na tuyaache matendo ya giza^o na

13:4 *Au "kuleta adhabu."

tuvae silaha za nuru.^a **13** Na tujuiendeshe kwa adabu^b kama wakati wa mchana, si katika karamu zenye vurugu* na ulivi, si katika ngono isiyo halali na mwenendo mpotovu,^{#c} si katika mizozo na wivu.^d **14** Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo,^e na msiwe mkipanga mapema kwa ajili ya tamaa za mwili.^f

14 Mkaribisheni mtu aliye na udhaifu katika imani yake,^g lakini msihukumu kuhusu maoni yanayotofautiana.* **2** Mtu mmoja ana imani ya kula kila kitu, lakini mtu aliye dhaifu hula mboga za majani tu. **3** Yule anayekula asimdharau yule asiyekula, na yule asiyekula asimhukumu yule anayekula,^h kwa maana Mungu amemkaribisha. **4** Wewe ni nani ili umhukumu mtumishi wa mwingine?ⁱ Kwa bwana wake yeye husimama au kuanguka.^j Kwa kweli, atasimamishwa, kwa maana Yehova* anaweza kumsimamisha.

5 Mtu mmoja anahukumu siku moja kuwa muhimu kuliko nyingine;^k mwingine anahukumu siku moja kuwa sawa na nyingine zote;^l kila mtu na asadikishwe kikamili katika akili yake mwenyewe. **6** Yule anayeishika siku huihshika kwa ajili ya Yehova.* Pia, yule anayekula, anakula kwa ajili ya Yehova,* kwa maana yeye humshukuru Mungu;^m na yule asiyekula, hali cha-

13:13 *Au "karamu za kupindukia."
[#]Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Wingi wa neno la Kigiriki *a-sel'gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. **14:1** *Au labda, "maswali ya ndani." **14:4, 6, 8, 11** *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 13

a 2Ko 6:4, 7
 Efe 6:11
 1Th 5:8

b 1Pe 2:12

c Efe 4:19
 1Pe 4:3

d 2Ko 12:20

e 1Ko 11:1
 Gal 3:27
 Efe 4:24

f Gal 5:16

SURA YA 14

g Ro 15:1
 1Th 5:14

h Kol 2:16

i Mt 7:1
 Yak 4:12

j 1Ko 4:4

k Gal 4:10

l Kol 2:16

m 1Ti 4:4

Safu ya 2

a 1Ko 10:31

b 1Ko 6:19, 20

c Zb 146:2
 1Pe 4:1, 2

d 1Th 4:14

e 1Th 5:10
 Ufu 1:17, 18

f Lu 6:37
 Ro 14:4

g Mdo 10:42
 2Ko 5:10

h Isa 49:18

i Isa 45:23

j Mhu 12:14
 Mt 12:36
 2Ko 5:10

k Mt 7:1

l Mt 18:6
 1Ko 8:9
 1Ko 10:32

m Mt 15:11
 Mdo 10:15
 1Ti 4:4

n Efe 5:2

kula kwa ajili ya Yehova,* na bado yeye humshukuru Mungu.^a **7** Hakuna hata mmoja wetu anayeishi kwa ajili yake mwenyewe tu,^b na hakuna yeyote anayekufa kwa ajili yake mwenyewe tu. **8** Kwa maana tukiishi, tunaishi kwa ajili ya Yehova,^{#c} na tukifa, tunakufa kwa ajili ya Yehova.* Basi tukiishi na tukifa, sisi ni wa Yehova.*^d **9** Kwa maana kwa kusudi hili Kristo alikufa na akawa hai tena, ili awe Bwana juu ya waliokufa na walio hai pia.^e

10 Lakini kwa nini unamhukumu ndugu yako?^f Au kwa nini pia unamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.^g **11** Kwa maana imeandikwa: "Kwa hakika kama ninavyoishi,^h asema Yehova,* 'kila goti litapigwa mbele zangu, na kila ulimi utakiri waziwazi kwa Mungu.'"ⁱ **12** Hivyo basi, kila mmoja wetu atatoa hesabu kwa Mungu kwa ajili yake mwenyewe.^j

13 Kwa hiyo tusiwe tukihukumiana tena,^k badala yake tuazimie kutoweka kikwazo au kizuizi mbele ya ndugu.^l **14** Ninajua, nami ninaamini katika Bwana Yesu kwamba hakuna kitu ambacho ndani yake chenyewe ni kichafu;^m isipokuwa tu mtu anapokiona kitu kuwa kichafu, kwa ke yeye hicho huwa kichafu. **15** Kwa maana ikiwa unamkasirisha ndugu yako kwa sababu ya chakula, wewe hutembe tena kulingana na upendo.ⁿ Kwa chakula chako usimwamamize* yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili

14:15 *Au "usimharibu."

yake.^a **16** Kwa hiyo, msiache mema mnayofanya yasemwe vibaya. **17** Kwa maana Ufalme wa Mungu haumaanishi kula na kunywa,^b bali unamaanisha uadilifu na amani na shangwe pamoja na roho takatifu. **18** Kwa maana yote anayemtumikia Kristo kwa njia hii anakubalika kwa Mungu naye ana kibali cha wanadamu.

19 Hivyo basi, na tufuatilie mambo yanayoleta amani^c na mambo ya kujengana.^d **20** Acheni kuibomoa kazi ya Mungu kwa ajili ya chakula tu.^e Ni kweli, vitu vyote ni safi, lakini ni vibaya* kwa mtu kula ikiwa itasababisha ki-kwazo.^f **21** Ni vema kutokula nyama au kunywa divai au kufanya jambo lolote ambalo litamkwaza ndugu yako.^g **22** Imani uliyo nayo, endelea kuwa nayo mbele za Mungu. Mwenye furaha ni mtu asiyejihukumu mwenyewe kwa yale anayokubali. **23** Lakini ikiwa ana shaka, yeye akila tayari atakuwa amehukumiwa kuwa mwenye hatia, kwa sababu hali kwa imani. Kwa kweli, kila kitu ambacho hakitokani na imani ni dhambi.

15 Basi, sisi tulio na nguvu tunapaswa kubeba udhaifu wa wale wasio na nguvu,^h na tusiwe tukijipendeza wenyewe.ⁱ **2** Kila mmoja wetu na ampendeze jirani yake kwa mema, ili kumjenga.^j **3** Kwa maana hata Kristo hakujipendeza mwenyewe,^k bali kama ilivyoandikwa: “Shutuma za wale wanaokushutumu zimeniangukia.”^l **4** Kwa maana mambo yote yaliyoandikwa zamani yaliandikwa ili

14:20 *Au “kosa.”

SURA YA 14

a 1Ko 8:10,11

b 1Ko 8:8

c Mt 5:9
Ro 12:18

d 1Ko 14:12
Ebr 10:24

e Ro 14:3
1Ko 8:11

f 1Ko 8:9

g Ro 14:13
1Ko 8:13
1Ko 10:24

SURA YA 15

h Ro 14:1
1Th 5:14

i 1Ko 10:24

j 1Ko 9:22
Flp 2:4

k Mk 10:45
Yoh 5:30

l Zb 69:9

Safu ya 2

a 1Ko 10:11
2Ti 3:16,17
2Pe 1:19

b Ro 5:3,4

c Zb 119:49,50
Ebr 3:6
1Pe 1:10

d 1Ko 1:10
2Ko 13:11
Flp 2:2
1Pe 3:8

e Flm 10,17

f Yoh 6:37

g Mt 15:24
Yoh 1:11

h Mwa 22:16-18
Zb 89:3

i Ro 9:23,24

j 2Sa 22:50
Zb 18:49

k Kum 32:43

l Zb 117:1

m Ufu 5:5

n Mwa 49:10

o Isa 11:1,10
Mt 12:21

p Isa 40:31

kutufundisha,^a ili kupitia uvumilivu wetu^b na kupitia faraja kutoka kwa Maandiko tuwe na tumaini.^c **5** Basi Mungu anayetoa uvumilivu na faraja na awezeshe ninyi miongoni mweni wenyewe kuwa na mtazamo uleule wa akili ambao Kristo Yesu alikuwa nao, **6** ili kwa umoja^d na kwa sauti moja* mumtukuze Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo.

7 Basi mkaribishane,^e kama vile Kristo pia alivyowakaribisha,^f kwa kusudi la kumtukuzwa Mungu. **8** Kwa maana ninawaambia kwamba Kristo alikuwa mhudumu wa wale waliotahiriwa^g kwa ajili ya ukweli wa Mungu, ili kuthibitisha ahadi ambazo Yeye aliwapa mababu zao,^h **9** na kwamba mataifa yamtukuze Mungu kwa sababu ya rehma yake.ⁱ Kama ilivyoandikwa: “Ndiyo sababu nitakukiri wewe waziwazi kati ya mataifa nami nitakwambia nyimbo za sifa.”^j **10** Tena anasema: “Furahini, enyi mataifa, pamoja na watu wake.”^k **11** Tena: “Msifuni Yehova,^{*} enyi mataifa yote, na watu wote wamsifu yeye.”^l **12** Na tena Isaya anasema: “Kutakuwa na mzizi wa Yese,^m yule anayesimama ili kutawala mataifa;ⁿ na mataifa yatamtumainia yeye.”^o **13** Mungu anayetoa tumaini na awajaze ninyi shangwe yote na amani kwa kumtegemea, ili tumaini lenu liongezoke* kwa nguvu za roho takatifu.^p

14 Ndugu zangu, sasa mimi mwenyewe nimesadiki kuwa-

15:6 *Tnn., “kinywa kimoja.” 15:7 *Au “muwakubali wengine.” 15:11 *Angalia Nyongeza A5. 15:13 *Au “lifurike.”

husu, kwamba ninyi pia mmejaa wema, mmejaa ujuzi wote, na kwamba mnaweza kuonyana.* **15** Hata hivyo, nimewaandikia waziwazi zaidi kuhusu mambo fulani, ili kuwakumbusha tena, kwa sababu ya fadhili zisizostahiliwa nilizopewa kutoka kwa Mungu **16** ili niwe mtumishi wa watu wote wa Kristo Yesu kwa mataifa.^a Ninafanya kazi takatifu ya habari njema ya Mungu,^b ili mataifa haya yawe toleo linalokubalika, lililotakaswa kwa roho takatifu.

17 Basi nina sababu ya kufurahi katika Kristo Yesu kuhusu mambo yanayohusiana na Mungu. **18** Kwa maana sitathubutu kusema kuhusu chochote isipokuwa yale ambayo Kristo amefanya kupitia mimi ili mataifa yatii, kwa maneno na matendo yangu, **19** kwa nguvu za ishara na mambo ya ajabu,^{*c} kwa nguvu za roho ya Mungu, hivi kwamba kutoka Yerusalemu na kuzunguka mpaka Ilirikamu nimehubiri kikamili habari njema kuhusu Kristo.^d **20** Kwa kweli, katika njia hii, nilikusudia kwamba nisingatangaze habari njema mahali ambapo jina la Kristo lilikuwa limetangazwa tayari, ili nisingenje juu ya msingi wa mtu mwingine; **21** bali, kama ilivyoandikwa: "Wale ambao hawajapata ujumbe wowote kuhusu wataona, na wale ambao hawajasikia wataelewa."^e

22 Pia hivyo ndiyo sababu nilizuiwa mara nyingi kuja kwenu. **23** Lakini sasa sina tena eneo ambalo halijaguswa kati-

15:14 *Au "kufundishana." 15:19 *Au "miujiza."

SURA YA 15

a Ro 11:13
Gal 2:7, 8

b Mdo 20:24

c Mdo 15:12
2Ko 12:12

d Mdo 21:18, 19

e Isa 52:15

Safu ya 2

a Mdo 19:21
Mdo 20:22

b 1Ko 16:1
2Ko 8:1-4
2Ko 9:2, 12

c Gal 6:6
Ebr 13:16

d 2Ko 1:11
Efe 6:18
Kol 4:3
1Th 5:25

e 2Th 3:1, 2

f Ro 15:26

ka maeneo haya, na kwa miaka mingi* nimetamani kuja kwenu. **24** Kwa hiyo, nikisafiri kwenda Uhispania, natumaini kwamba nitawaona na mtanisindikiza umbali fulani, baada ya mimi kufurahia ushirika wenu kwa muda. **25** Lakini sasa ninakaribia kusafiri kwenda Yerusalemu kuwahudumia watakatifu.^a **26** Kwa maana wale walio Makedonia na Akaya wamependewa kushiriki vitu vyao kwa kuwatolea mchango fulani walio maskini kati ya watakatifu huko Yerusalemu.^b **27** Kweli, wamependewa kufanya hivyo, na kwa hakika walikuwa wadani kwao; kwa maana ikiwa mataifa wameshiriki mambo yao ya kiroho, wao pia wana deni la kuwahudumia kwa vitu vyao vya kimwili.^c **28** Basi nikimaliza jambo hili na kuwafikishia mchango huu* salama, nitandoka na kupitia kwenu nikielekea Uhispania. **29** Isitoshe, najua kwamba nitakapokuja kwenu nitakuja nikiwa na kipimo kamili cha baraka kutoka kwa Kristo.

30 Sasa ninawahimiza ninyi, akina ndugu, kupitia Bwana wetu Yesu Kristo na kupitia upendo wa roho, kwamba mjikaze pamoja nami katika kusali kwa Mungu kwa ajili yangu,^d **31** ili nikombolewe^e kutoka kwa wale wasio waamini huko Yudea na kwamba huduma yangu kwa ajili ya Yerusalemu ikubalike kwa watakatifu,^f **32** ili kwa mapenzi ya Mungu nije kwenu nikiwa na shangwe na kuburudishwa pamoja nanyi.

15:23 *Au labda, "kadhaa." 15:28 *Tnn., "tunda hili."

33 Mungu anayetoa amani na awe pamoja nanyi nyote.^a Amina.

16 Ninamtambulisha* kwenye Fibi dada yetu, ambaye ni mhudumu wa kutaniko lililo huko Kenkrea,^b 2 ili mumkaribishe katika Bwana kwa njia inayowastahili watakatifu, na kumpa msada wowote ambao huenda akahitaji,^c kwa maana yeye pia alikuwa mtetezi wa wengi, kutia ndani mimi mwenyewe.

3 Wapeni salamu zangu Priska na Akila,^d wafanyakazi wenzangu katika Kristo Yesu, **4** ambao wamehatarisha uhai wao kwa ajili yangu,^e na si mimi tu ninayewashukuru bali pia makutaniko yote ya mataifa. **5** Pia salimuni kutaniko lililo katika nyumba yao.^f Msalimuni Epaineto mpendwa wangu, aliye matunda ya kwanza ya Asia kwa ajili ya Kristo. **6** Msalimuni Maria, ambaye amefanya kazi kwa bidii kwa ajili yenu. **7** Wasalimuni Androniko na Yunia, watu wangu wa ukoo^g na wafungwa wenzangu, ambao ni watu wanaojulikana kwa mitume na ambao wamekuwa katika muungano na Kristo muda mrefu zaidi yangu.

8 Mpeni salamu zangu Ampliato, mpendwa wangu katika Bwana. **9** Salimuni Urbano mfanyakazi mwenzetu katika Kristo, na Stako mpendwa wangu. **10** Msalimuni Apele, aliyekubaliwa katika Kristo. Wasalimuni wale wa nyumbani mwa Aristobulo. **11** Msalimuni Herodioni, mtu wangu wa ukoo. Wasalimuni wale wa

16:1 *Au "Ninampendekeza." 16:4 *Au "nafsi yangu."

SURA YA 15

a 1Ko 14:33
Flp 4:9

SURA YA 16

b Mdo 18:18

c Ro 12:13
1Yo 3:17

d Mdo 18:2
Mdo 18:24, 26
2Ti 4:19

e 1Yo 3:16

f 1Ko 16:19
Kol 4:15
Flm 2

g Ro 16:11

Safu ya 2

a Mt 7:15
Tit 3:10
2Yo 10

b 1Ko 14:20

c Mwa 3:15
Ebr 2:14

nyumbani mwa Narkiso walio katika Bwana. **12** Wasalimuni Trifaina na Trifosa, wanawake wanaofanya kazi kwa bidii katika Bwana. Msalimuni Persisi mpendwa wetu, kwa maana mwanamke huyo amefanya kazi kwa bidii katika Bwana. **13** Salimuni Rufo aliyechaguliwa katika Bwana, na mama yake ambaye pia ni mama yangu. **14** Wasalimuni Asinkrito, Flegoni, Hermesi, Patroba, Hermasi, na akina ndugu walio pamoja nao. **15** Wasalimuni Filologo na Yulia, Nerea na dada yake, na Olimpa, na watakatifu wote walio pamoja nao. **16** Salimianeni kwa busu takatifu. Makutaniko yote ya Kristo yanawasalimu ninyi.

17 Sasa ninawahimiza ninyi, akina ndugu, waangalie ni wale wanaosababisha migawanyiko na kuweka vikwazo kinyume cha fundisho ambalo mmejifunza, nanyi mjiepushe nao.^a **18** Kwa maana watu wa namna hiyo ni watumwa, si wa Bwana wetu Kristo, bali wa hamu* yao wenyewe, na kwa maneno laini na maneno ya kusifusifu wao huishawishi mioyo ya wasiotambua. **19** Utii wenu umejulikana na watu wote, basi ninashangilia kwa sababu yenu. Hata hivyo, ninataka muwe na hekima kuhusu yaliyo mema, lakini wasio na hatia kuhusu yaliyo maovu.^b **20** Kwa upande wake, Mungu anayetoa amani atamponda Shetani^c chini ya miguu yenu hivi karibuni. Fadhili zizizostahiliwa za Bwana wetu Yesu na ziwe pamoja nanyi.

16:18 *Au "matumbo."

21 Timotheo, mfanyakazi mwenzangu anawasalimu ninyi, na pia Lukio, Yasoni, na Sosipata, watu wangu wa ukoo.^a

22 Mimi, Tertio, ambaye ni-meandika barua hii, ninawasalimu ninyi katika Bwana.

23 Gayo,^b aliyenikaribisha mimi na kutaniko lote, anawasalimu ninyi. Erasto, mweka hazina* wa jiji, anawasalimu ninyi, na pia Kwarto, ndugu yake. **24** *—

25 Sasa kwa Yule anayeweza kuwaimarisha ninyi kuli-

16:23 *Au “msimamizi.” **16:24** *Angalia Nyongeza A3.

SURA YA 16

a Ro 16:7

b 1Ko 1:14

Safu ya 2

a Efe 1:9-12
Kol 1:26, 27

b Ro 11:33

ngana na habari njema nina-
yotangaza na kuhubiriwa kwa
Yesu Kristo, kulingana na ufu-
nuo wa siri takatifu^a amba-
yo ilikuwa imefichwa ta-
ngu nyakati za zamani **26** la-
kini sasa imeonyeshwa wazi*
na kujulishwa kupitia Maa-
ndiko ya kinabii kati ya ma-
taifa yote kulingana na amri
ya Mungu anayedumu milele,
ili kuendeleza utii kwa imani;
27 kwa Mungu, ambaye peke
yake ndiye mwenye hekima,^b
kuwe na utukufu kupitia Yesu
Kristo milele. Amina.

16:26 *Au “imefunuliwa.”

BARUA YA KWANZA KWA

WAKORINTHO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1-3)
Paulo amshukuru Mungu kwa sababu
ya Wakorintho (4-9)
Wahimizwa kuwa na umoja (10-17)
Kristo, nguvu na hekima ya
Mungu (18-25)
Kujisifu tu katika Yehova (26-31)
- 2 Paulo ahubiri huko Korintho (1-5)
Ubora wa hekima ya Mungu (6-10)
Tofauti kati ya mtu wa kiroho na mtu wa
kimwili (11-16)
- 3 Bado Wakorintho ni wa kimwili (1-4)
Mungu hufanya ikue (5-9)
Wafanyakazi wenzi wa Mungu (9)
Jengeni kwa vifaa visivyoshika
moto (10-15)
Ninyi ni hekalu la Mungu (16, 17)
Hekima ya ulimwengu ni upumbavu
kwa Mungu (18-23)
- 4 Wasimamizi wanapaswa kuwa
waaminifu (1-5)

- Unyenyekevu wa wahudumu
Wakristo (6-13)
“Msipite mambo yaliyoandikwa” (6)
Wakristo ni tamasha (9)
Paulo awajali watoto wake wa
kiroho (14-21)
- 5 Kisa cha uasherati (1-5)
Chachu kidogo huchachisha donge
lote (6-8)
Mtu mwovu aondolewe (9-13)
 - 6 Kesi miongoni mwa akina ndugu
Wakristo (1-8)
Wale ambao hawataurithi Ufalme (9-11)
Mtukuzeni Mungu katika miili
yenu (12-20)
“Ukimbieni uasherati!” (18)
 - 7 Ushauri kwa waseja na waliofunga
ndoa (1-16)
Baki katika hali uliyokuwa nayo
ulipoitwa (17-24)
Waseja na wajane (25-40)

- Faida za kuwa mseja (32-35)
Funga ndoa “katika Bwana tu” (39)
- 8 Kuhusu chakula kinachotolewa kwa sanamu (1-13)
Kwetu kuna Mungu mmoja tu (5, 6)
- 9 Mfano wa Paulo akiwa mtume (1-27)
“Hupaswi kumfunga kinywa ng’ombe dume” (9)
‘Ole wangu nisipohubiri!’ (16)
Kuwa vitu vyote kwa watu wote (19-23)
Kujidhibiti katika mbio za uzima (24-27)
- 10 Vielelezo vya kuonya kutokana na historia ya Israeli (1-13)
Onyo dhidi ya ibada ya sanamu (14-22)
Meza ya Yehova, meza ya roho waovu (21)
Uhuru na kuwafikiria wengine (23-33)
“Fanyeni mambo yote kwa utukufu wa Mungu” (31)
- 11 “Iweni waigaji wangu” (1)
Ukichwa na kufunika kichwa (2-16)
Kuahimisha Mlo wa Jioni wa Bwana (17-34)
- 12 Zawadi za roho (1-11)
Mwili mmoja, viungo vingi (12-31)
- 13 Upendo—njia bora zaidi (1-13)
- 14 Zawadi za unabii na lugha (1-25)
Mikutano ya Kikristo yenye utaratibu (26-40)
Sehemu ya wanawake katika kutaniko (34, 35)
- 15 Ufufuo wa Kristo (1-11)
Ufufuo, msingi wa imani (12-19)
Ufufuo wa Kristo unatoa uhakikisho (20-34)
Mwili wa nyama, mwili wa kiroho (35-49)
Kutoweza kufa na kutoweza kuharibika (50-57)
Kuwa na mengi ya kufanya katika kazi ya Bwana (58)
- 16 Mchango kwa ajili ya Wakristo huko Yerusalemu (1-4)
Mipango ya safari za Paulo (5-9)
Mipango ya ziara za Timotheo na Apolo (10-12)
Himizo na salamu (13-24)

1 Paulo, aliyeitwa kuwa mtume^a wa Kristo Yesu kupitia mapenzi ya Mungu, na Sosthene ndugu yetu, **2** kwa kutaniko la Mungu lililo huko Korintho,^b kwenu ninyi ambao mmetakaswa katika muungano na Kristo Yesu,^c mlioi-twa kuwa watakatifu, pamoja na wale wote ambao kila mahali wanaliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo,^d Bwana wao na wetu:

3 Na muwe na fadhili zizozostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

4 Sikuzote ninamshukuru Mungu wangu kwa ajili yenu kwa sababu ya fadhili zizozostahiliwa za Mungu mli-zopewa katika Kristo Yesu;

SURA YA 1

a Mdo 9:15

b Mdo 18:1

c 1Ko 6:11
Ebr 9:13,14d Mt 12:18,21
Mdo 4:12

Safu ya 2

a Kol 1:9

b Mdo 18:5

c Lu 17:29,30
2Th 1:7
1Pe 1:7d 1Ko 4:5
1Ko 5:5
Ufu 1:10

e Kum 7:9

5 kwa kuwa katika yeye mmetajirishwa katika kila jambo, katika uwezo kamili wa ku-sema na katika ujuzi kamili,^a **6** kama vile ushahidi kumhusu Kristo^b ulivyofanywa kuwa imara miongoni mweni, **7** ili msipungukiwe hata kidogo katika zawadi yoyote, huku mkisubiri kwa hamu ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo.^c **8** Yeye pia atawafanya ninyi muwe imara mpa-ka mwisho, ili msiwe na shtaka lolote katika siku ya Bwana wetu Yesu Kristo.^d **9** Mungu ni mwaminifu,^e aliyewaita muwe na ushirika pamoja na Mwana wake, Yesu Kristo Bwana wetu.

10 Sasa ninawahimiza ninyi, akina ndugu, kupitia

jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mseme kwa upatano, na kwamba kusiwe na migawanyiko kati yenu,^a bali kwamba muunganishwe kabisa katika akili ileile na njia ileile ya kufikiri.^b **11** Kwa maana baadhi ya watu wa nyumba ya Kloe wamenijulisha kuwahusu ninyi ndugu zangu, kwamba kuna ugomvi kati yenu. **12** Ninaloamaanisha ni hili, kwamba kila mmoja wenu anasema: "Mimi ni wa Paulo," "Lakini mimi ni wa Apolo,"^c "Lakini mimi ni wa Kefa,"* "Lakini mimi ni wa Kristo." **13** Je, Kristo amegawanyika? Paulo hakuuawa kwenye mti kwa ajili yenu, siyoy? Au je, mlibatizwa katika jina la Paulo? **14** Nina-mshukuru Mungu kwa kuwa sikumbatiza hata mmoja wenu isipokuwa Krispo^d na Gayo,^e **15** ili yeyote asiseme kwamba mlibatizwa katika jina langu. **16** Ndiyo, niliibatiza pia nyumba ya Stefana.^f Kuhusu wale wengine, sijui kama nilimbati-za mwingine yeyote. **17** Kwa maana Kristo alinituma, si kubatiza, bali kutangaza habari njema;^g na si kwa maneno ya hekima,* ili mti wa mateso[#] wa Kristo usifanywe kuwa kitu kisicho na maana.

18 Kwa maana maneno kuhusu mti wa mateso[#] ni upumbavu kwa wale wanaoangamia,^h lakini kwetu sisi tunaokolewa, ni nguvu za Mungu.ⁱ **19** Kwa maana imeandikwa: "Nitaiangamiza hekima ya watu wenye hekima, nami nitaitakataa* akili ya watu we-

1:12 *Pia anaitwa Petro. 1:17 *Au "ujanja." 1:17, 18 #Angalia Kamusi, uku. 2012. 1:19 *Au "nitaiweka kando."

SURA YA 1

a Ro 16:17

b Ro 15:5, 6
2Ko 13:11
Efe 4:1, 3
Flp 2:2c Mdo 18:24
1Ko 3:4, 5
1Ko 3:21-23

d Mdo 18:8

e Ro 16:23

f 1Ko 16:15

g Mdo 9:15

h Mdo 17:18
1Ko 2:14

i Ro 1:16

Safu ya 2

a Isa 29:14

b Lu 10:21

c Kol 2:8

d 1Ko 2:14
1Ko 3:18e Mt 12:38
Lu 11:29

f Mdo 17:32

g Kol 2:3

h 2Ko 13:4

i Mdo 4:13

j Yoh 7:48
Yak 2:5

k Mt 11:25

nye akili."^a **20** Yuko wapi mtu mwenye hekima? Yuko wapi mwandishi? Yuko wapi anayebishania maneno katika mfumo huu wa mambo?[#] Je, Mungu hakuifanya hekima ya ulimwengu iwe upumbavu? **21** Kwa kuwa, katika hekima ya Mungu, ulimwengu haukumjua Mungu^b kupitia hekima yake,^c Mungu alipenda kuwao-koa wale wanaoamini kupitia upumbavu^d wa ujumbe unao-hubiriwa.

22 Kwa maana Wayahudi wanaomba ishara^e na Wagiriki wanatafuta hekima; **23** lakini sisi tunamhubiri Kristo aliyuawa kwenye mti, kwa Wayahudi ni sababu ya kujikwaa lakini kwa mataifa ni upumbavu.^f **24** Hata hivyo, kwa wale walioitwa, Wayahudi na Wagiriki, Kristo ni nguvu za Mungu na hekima ya Mungu.^g **25** Kwa sababu kitu kipumbavu cha Mungu ni chenye hekima kuliko wanadamu, na kitu dhaifu cha Mungu ni chenye nguvu kuliko wanadamu.^h

26 Kwa maana akina ndugu, mnaona mwito wake kwenye hekima kwa njia ya kimwili,^{*j} si wengi wenye nguvu, si wengi wa kutoka familia mashuhuri,^j **27** bali Mungu alivichagua vitu vipumbavu vya ulimwengu ili awaabishe watu wenye hekima; na Mungu alivichagua vitu dhai-ifu vya ulimwengu, ili aviaibishe vitu vyenye nguvu;^k **28** na Mungu alivichagua vitu vinyonge vya ulimwengu na vitu vinavyodharauliwa, vitu

1:20 *Yaani, mtaalamu wa Sheria. #Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo." 1:26 *Au "kwa viwango vya wanadamu."

ambavyo si kitu, ili kuvifanya vitu ambavyo ni kitu visiwe kitu,^a **29** ili mtu yeyote asijisifu* machoni pa Mungu. **30** Lakini ni kwa sababu yake kwamba ninyi mko katika muungano na Kristo Yesu, ambaye kwetu amekuwa hekima kutoka kwa Mungu, pia uadilifu^b na utakaso^c na kuachiliwa huru kupitia fidia,^d **31** ili iwe kama ilivyoandikwa: “Yule anayejisifu, na ajisifu katika Yehova.”^e

2 Kwa hiyo, nilipokuja kwenu, akina ndugu, sikuja na maneno mengi^f au hekima nikiwatangazia siri takatifu^g ya Mungu. **2** Kwa maana niliamua kutojua kitu chochote kati yenu isipokuwa Yesu Kristo, naye akiwa ameuawa kwenye mti.^h **3** Nami nilikuja kwenu nikiwa dhaifu, mwenye woga na nikitetemeka sana; **4** na katika maneno yangu na mambo niliyohubiri sikutumia maneno ya kushawishi yenye hekima bali wonyesho wa roho na nguvu,ⁱ **5** ili imani yenu iwe, si katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.

6 Basi tunazungumza kuhusu hekima kati ya wale ambao ni wakomavu,^j lakini si hekima ya mfumo huu wa mambo* wala ile ya watawala wa mfumo huu wa mambo, ambao watapitilia mbali.^k **7** Bali tunazungumza kuhusu hekima ya Mungu katika siri takatifu,^l hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliagiza awali kabla ya mifumo

1:29 *Tnn., “mwili wowote usijisifu.”
1:31 *Angalia Nyongeza A5. 2:6, 8
*Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mfumo wa mambo.”

SURA YA 1

a 1Ko 2:6

b Ro 10:4
2Ko 5:21c Yoh 17:19
Ebr 10:10d Ro 3:24
Kol 1:13, 14e Yer 9:24
2Ko 10:17

SURA YA 2

f 1Ko 1:17

g Efe 3:5, 6
Kol 2:2

h Gal 6:14

i Ro 15:18, 19
1Ko 4:20
1Th 1:5j 1Ko 14:20
Efe 4:13
Ebr 5:14

k 1Ko 15:24

l Ro 16:25, 26
Efe 3:8, 9

Safu ya 2

a Yoh 7:48
Mdo 13:27, 28

b Isa 64:4

c Mt 16:17
Mk 4:11
Efe 3:5
ZTi 1:9, 10
1Pe 1:12d Yoh 14:26
1Yo 2:27

e Ro 11:33

f Yoh 15:26

g Kol 2:8

h Yoh 16:13

i Ro 8:5

ya mambo kwa ajili ya utukufu wetu. **8** Hakuna mtawala hata mmoja wa mfumo huu wa mambo* aliyejua hekima hii,^a kwa maana kama wangejua hawangemuaa[#] Bwana mwenye utukufu. **9** Lakini kama ilivyoandikwa: “Jicho halijao na na sikio halijasikia, wala hayajawaziwa katika moyo wa mwanadamu mambo ambayo Mungu amewatayarishia wale wanaompenda.”^b **10** Kwa maana Mungu ameyafunua kwetu^c kupitia roho yake,^d kwa maana roho huchunguza ndani ya mambo yote, hata mambo mazito* ya Mungu.^e

11 Kwa maana ni nani kati ya wanadamu anayejua mambo ya mwanadamu isipokuwa roho ya mwanadamu iliyondani yake? Vivyo hivyo, hakuna ambaye ameyajua mambo ya Mungu, isipokuwa roho ya Mungu. **12** Basi, sisi hatukupokea roho ya ulimwengu, bali tulipokea roho inayotoka kwa Mungu,^f ili tuyajue mambo ambayo Mungu ametupatia kwa fadhili. **13** Mambo hayo tunayasema pia, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya binadamu,^g bali kwa yale yanayofundishwa kwa roho,^h tunapofafanua* mambo ya kiroho kwa maneno ya kiroho.

14 Lakini mtu wa kimwili hayakubali* mambo ya roho ya Mungu, kwa maana hayo ni upumbavu kwake; naye hawazi kuyajua, kwa sababu yanachunguzwa kiroho. **15** Hata hivyo, mtu wa kiroho huchunguza mambo yote,ⁱ laki-

2:8 [#]Au “hawangemtundika kwenye mti.” 2:10 *Au “yenye kina.” 2:13 *Au “tunapounganisha.” 2:14 *Au “haya-pokei.”

ni yeye mwenyewe hachunguzwi na mwanadamu yeyote. **16** Kwa maana “ni nani amejua akili ya Yehova,* ndipo amfundishe?”^a Lakini sisi tunayo akili ya Kristo.^b

3 Basi akina ndugu, mimi si kuweza kuzungumza nanyi kama watu wa kiroho,^c bali kama watu wa kimwili, kama watoto^d katika Kristo. **2** Niliwalisha maziwa, si chakula kigumu, kwa maana mlikuwa bado hamna nguvu za kutosha. Kwa kweli, hata sasa hamna nguvu za kutosha,^e **3** kwa maana bado ninyi ni wa kimwili.^f Kwa kuwa kuna wivu na mizozo kati yenu, je, ninyi si wa kimwili^g na je, hamtembei kama wanadamu w navyotembea? **4** Kwa maana mtu mmoja anaposema, “Mimi ni wa Paulo,” naye mwingine anasema, “Mimi ni wa Apolo,”^h je, hamfanyi kama wanadamu tu?

5 Basi, Apolo ni nani? Ndiyo, Paulo ni nani? Wahudumu' ambao kupitia wao mlikuja kuwa waamini, kama vile Bwana alivyomwezesha kila mmoja. **6** Mimi nilipanda,ⁱ Apolo akatia maji,^k lakini Mungu akaendelea kuikuza, **7** hivi kwamba anayepanda si kitu wala anayetia maji, bali Mungu anayeikuza.^l **8** Basi anayepanda na anayetia maji ni kitu kimoja,* lakini kila mtu atapokea thawabu yake kulingana na kazi yake mwenyewe.^m **9** Kwa maana sisi ni wafanyakazi wenzi wa Mungu. Ninyi ni shamba la Mungu linalolimwa, jengo la Mungu.ⁿ

2:16 *Angalia Nyongeza A5. 3:8 *Au “wana kusudi moja.”

SURA YA 2

a Isa 40:13

b Ro 15:5

SURA YA 3

c 1Ko 2:15

Kol 1:9

d 1Ko 14:20

e Ebr 5:12-14

f Ro 8:7, 8

g Gal 5:19, 20

h Mdo 18:24, 25

i 2Ko 3:5, 6

Kol 1:23

1Ti 1:12

j Mdo 18:4

k Mdo 18:26-28

Mdo 19:1

l Ro 9:16

m Ro 2:6

1Ko 4:5

Ufu 22:12

n Efe 2:22

1Pe 2:5

Safu ya 2

a Ro 15:20

Ebr 6:1

b Zb 118:22

Isa 28:16

Mt 21:42

Efe 2:20

1Pe 2:6

c 1Pe 4:12

d 2Ko 6:16

Efe 2:21

1Pe 2:5

e 1Ko 6:19

f 1Pe 2:5

10 Kulingana na fadhili zisizostahiliwa za Mungu nilizopewa, niliweka msingi,^a nikiwa mjenzi mkuu mwenye ustadi,* hata hivyo, mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mmoja na aendeleo kuanzalia jinsi anavyojenga juu yake. **11** Kwa maana hakuna mtu yeyote anayeweza kuweka msingi mwingine wowote zaidi ya ule uliowekwa, ambao ni Yesu Kristo.^b **12** Basi yeyote akijenga juu ya msingi huo dhahabu, fedha, mawe ya thamani, mbao, nyasi kavu, au majani makavu, **13** kazi ya kila mmoja itaonekana jinsi ilivyo,* kwa maana ile siku itaifichua, kwa sababu itafunuliwa kupitia moto,^c na moto wenyewe utaonyesha jinsi kila mmoja alivyojenga. **14** Ikiwa kazi ya yeyote aliyajenga juu yake itabaki, atapokea thawabu; **15** ikiwa kazi ya yeyote itateketea, atapata hasara, lakini yeye mwenyewe ataokolewa; hata hivyo, itakuwa ni kama kupitia moto.

16 Je, hamjui kwamba ninyi ni hekalu la Mungu,^d na kwamba roho ya Mungu inakaa ndani yenu?^e **17** Yeyote akiliangamiza hekalu la Mungu, Mungu atamwangamiza; kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, nanyi ni hekalu hilo.^f

18 Mtu yeyote asijidanganye: Ikiwa yeyote miongoni mweni anafikiri ana hekima katika mfumo huu wa mambo,* acheni awe mpu mbavu ili awe na hekima. **19** Kwa maana hekima ya

3:10 *Au “msimamizi wa kazi mwenye hekima.” 3:13 *Tnn., “itafunuliwa.” 3:18 *Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mfumo wa mambo.”

ulimwengu huu ni upumbavu kwa Mungu, kwa kuwa imeandikwa: “Yeye huwanasa wenyewe hekima katika ujanja wao wenyewe.”^a **20** Na tena: “Yehova* anajua kwamba kufikiri kwa watu wenyewe hekima ni ubatili.”^b **21** Basi yeyote asijisifu katika watu; kwa maana vitu vyote ni vyenu, **22** iwe ni Paulo au Apolo au Kefa*^c au ulimwengu au uzima au kifo au mambo yaliyopo sasa au mambo yatakayokuja, vitu vyote ni vyenu; **23** nanyi ni wa Kristo;^d naye Kristo ni wa Mungu.

4 Mtu anapaswa kutuona kuwa wahudumu* wa Kristo na wasimamizi wa siri takatifu za Mungu.^e **2** Katika hali hii, kinachotarajiwa katika wasimamizi ni kupatwa wakiwa waaminifu. **3** Basi kwangu si muhimu sana ku-chunguzwa na ninyi au na mahakama.* Hata mimi siji-chunguzi mwenyewe. **4** Kwa maana sioni kosa lolote dhidi yangu mwenyewe. Lakini hilo halithibitishi kuwa mimi ni mwadilifu; anayenichunguza ni Yehova.*^f **5** Kwa hiyo, msihukumu^g chochote kabla ya wakati unaofaa, mpaka Bwana aje. Ataleta mambo ya siri yaliyo ya giza kwenye nuru na pia kujulisha nia za muiyo, na ndipo kila mtu atakapopokea sifa yake kutoka kwa Mungu.^h

6 Basi, akina ndugu, mambo haya nimeyatimia* kujihusu mimi mwenyewe na Apoloⁱ kwa faida yenu, ili kupitia sisi

3:20; 4:4 *Angalia Nyongeza A5. 3:22 *Pia anaitwa Petro. 4:1 *Au “wasaidizi.” 4:3 *Au “baraza la wanadamu.” 4:6 *Au “nimeyamisha.”

SURA YA 3

a Ayu 5:13

b Zb 94:11

c 1Ko 1:12

d Yoh 17:9
2Ko 10:7

SURA YA 4

e Mt 13:11
Ro 16:25, 26f Met 21:2
Ro 14:10
Ebr 4:13

g Mt 7:1

h Met 10:9
2Ko 10:18
1Ti 5:24, 25

i 1Ko 1:12

Safu ya 2

a Ro 12:3
2Ko 12:20
3Yo 9

b Yoh 3:27

c Ufu 20:4, 6

d 2Ti 2:12
Ufu 3:21e Ro 8:36
1Ko 15:32
2Ko 6:4, 9

f Ebr 10:33

g 1Ko 3:18

h Flp 4:12

i 2Ko 11:27

j Mdo 14:19
Mdo 23:2
2Ko 11:24k Mdo 18:3
Mdo 20:34
1Th 2:9l Ro 12:14
1Pe 3:9

m Mt 5:44

n 1Pe 2:23

mjifunze kanuni hii: “Msiipite mambo yaliyoandikwa,” ili msiwe na kiburi,^a na kumpe-ndelea mtu mmoja kuliko mwingine. **7** Kwa maana ni nani anayekufanya wewe kuwa tofauti na mwingine? Kwa kweli, una nini ambacho hukupokea?^b Basi, ikiwa kwa kweli ulikipokea, kwa nini unajisifu kana kwamba hukupokea?

8 Je, tayari mmetosheka? Je, tayari ninyi ni matajiri? Je, mmeanza kutawala mkiwa wafalme^c bila sisi? Ninatamani sana kwamba muwe mmeanza kutawala mkiwa wafalme, ili sisi pia tutawale pamoja nanyi tukiwa wafalme.^d **9** Kwa maana ninaona kwamba Mungu ametuweka sisi mitume mwisho katika wonyesho wa hadharani kama watu waliohukumiwa kifo,^e kwa sababu tumekuwa tamasha kwa ulimwengu,^f na kwa malaka, na kwa wanadamu. **10** Sisi ni wapumbavu^g kwa sababu ya Kristo, lakini ninyi ni wenyewe busara katika Kristo; sisi ni dhaifu, lakini ninyi ni wenyewe nguvu; ninyi mnaheshimika, lakini sisi hatuheshimiki. **11** Mpaka saa hii tunape-ndelea kuwa na njaa^h na kiuⁱ na kukosa mavazi ya kutosha* na kupigwa^{aj} na kuya bila makao **12** na kufanya kazi ya taabu, tukifanya kazi kwa mikono yetu wenyewe.^k Tunapotukanwa, tunabariki;^l tunapoteswa, tunavumilia kwa subira;^m **13** tunapochongewa, tunajibu kwa upole;ⁿ tumekuwa kama takataka ya ulimwengu, uchafu wa vitu vyote, mpaka sasa.

4:11 *Tnn., “kuwa uchi.” ^aAu “kupigwa huku na huku.” 4:13 *Tnn., “tunasihii.”

14 Ninaandika mambo haya, si ili niwaaibishe, bali niwao-nye kama watoto wangu wape-ndwa. **15** Kwa maana inga-wa huenda mkawa na wale-zi* 10,000 katika Kristo, ha-kika hamna baba wengi; kwa maana katika Kristo Yesu mimi nimekuwa baba yenu ku-pitia habari njema.^a **16** Kwa hiyo, ninawasihi, iweni waiga-ji wangu.^b **17** Ndiyo sababu ninamtuma Timotheo kwenu, kwa kuwa yeye ni mtoto wa-angu mpendwa na mwaminifu katika Bwana. Atawakumbu-sha njia* zangu kuhusiana na Kristo Yesu,^c kama vile nina-vyofundisha kila mahali kati-ka kila kutaniko.

18 Wengine wamekuwa na kiburi wakidhani kwamba siji kwenu. **19** Lakini nita-kuja kwenu hivi karibuni, Ye-hova* akipenda, nami nita-jua, si maneno ya wale walio na kiburi, bali nguvu zao. **20** Kwa maana Ufalme wa Mu-ngu si maneno tu bali ni ngu-vu. **21** Mngependa nini? Je, nije kwenu nikiwa na fimbo^d au kwa upendo na upole wa roho?

5 Kwa kweli kuna habari kwamba kuna uasherati*^e miongoni mwenu, tena uashe-rati* ambao haujatokea hata miongoni mwa mataifa—mwa-namume kuishi^f na mke wa baba yake.^f **2** Na je, ninyi mnajivunia jambo hilo? Je, ham-paswi kuomboleza^g ili mtu aliyefanya kitendo hicho a-ondolewe miongoni mwenu?^h **3** Ingawa sipo katika mwili,

4:15 *Au "watumzaji." 4:17 *Au "mbi-nu." 4:19 *Angalia Nyongeza A5. 5:1 *Neno la Kigiriki *pornei*'a. Angalia Ka-musi, uku. 2012. ^aTnn., "kuwa."

SURA YA 4

a Gal 4:19
1Th 2:11b 1Ko 11:1
Flp 3:17
1Th 1:6

c 2Ti 1:13

d 2Ko 13:10

SURA YA 5

e Efe 5:3

f Law 18:8

g 2Ko 7:9

h 1Ko 5:13
2Yo 10

Safu ya 2

a 1Ti 1:20

b 1Ko 1:8

c 1Ko 15:33
Gal 5:9
2Ti 2:16, 17

d Yoh 1:29

e 1Pe 1:19, 20
Ufu 5:12

f Kut 13:7

g 1Yo 2:17

h Yoh 17:15

i Hes 16:25, 26
Ro 16:17
2Yo 10

j Efe 5:5

k Kum 21:20, 21
1Pe 4:3l 1Ko 6:9, 10
Gal 5:19-21

nipo katika roho, tayari ni-memhukumu mtu huyo amba-ye amefanya tendo hilo, kana kwamba nipo pamoja nanyi.

4 Mnapokusanyika pamoja katika jina la Bwana wetu Yesu, na kujua kwamba nipo nanyi katika roho pamoja na nguvu za Bwana wetu Yesu, **5** lazima mumkabidhi mtu wa namna hiyo kwa Shetani^a kwa ajili ya kuangamizwa kwa mwili, ili roho iokolewe katika siku ya Bwana.^b

6 Kujisifu kwenu hakufai. Je, hamjui kwamba chachu* kidogo huchachisha donge lote?^c **7** Ondoeni chachu ya zamani, ili muwe donge jipya, kwa kuwa ninyi hamna cha-chu. Kwa maana, kwa kweli, Kristo mwanakondoo wetu wa Pasaka^d ametolewa dhabihu.^e **8** Basi na tufanye sherehe,^f si kwa chachu ya zamani, wala kwa chachu ya ubaya na uovu, bali kwa mikate isiyu na cha-chu ya unyoofo na kweli.

9 Katika barua yangu nili-waandikia mwache kushiri-kiana* na waasherati,^g **10** si kumaanisha waasherati^g wa ulimwengu huu^g au watu we-nye pupa na wanyang'anyi au waabudu-sanamu. Kama inge-kuwa hivyo, kwa kweli inge-wabidi mwondoke katika uli-mwengu.^h **11** Lakini sasa ni-nawaandikia mwache kushiri-kiana*ⁱ na mtu yeyote anayeitwa ndugu ambaye ni mwasherati^g au mtu mwenye pupa^j au anayeabudu sana-mu au mtukanaji^Δ au mlevi^k au mnyang'anyi,^l hata msile

5:6 *Au "hamira." 5:9, 11 *Au "kucha-ngamana." 5:9-11 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Uasherati." 5:11 ^ΔAu "mtu anayetumia maneno machafu."

chakula pamoja na mtu wa namna hiyo. **12** Kwa maana inanihusu nini kuwahukumu wale walio nje? Je, ninyi hamwahukumu wale walio ndani, **13** huku Mungu akiwahukumu wale walio nje?^a “Mwondoeni mtu mwovu miongoni mwenu.”^b

6 Je, kuna yeyote kati yenu aliye na ugomvi na mwenzake^c atakayethubutu kwenda mahakamani mbele ya watu wasio waadilifu, na si mbele ya watakatifu? **2** Au je, hamjui kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu?^d Na ikiwa ninyi mtauhukumu ulimwengu, je, hamna uwezo wa kuamua mambo mado-go sana? **3** Je, hamjui kwamba tutawahukumu malaika?^e Basi, kwa nini isiwe mambo ya maisha haya? **4** Basi, ikiwa mna mambo ya maisha haya yanayohitaji kuamuliwa,^f je, mnawaweka watu wanaodharauliwa na kutaniko kuwa waamuzi? **5** Ninasema ili kuwatia ninyi aibu. Je, hakuna hata mtu mmoja mwenye hekima miongoni mwenu anayeweza kuhukumu kati ya ndugu zake? **6** Badala yake ndugu anaenda mahakamani kumshtaki ndugu, na tena mbele ya wasio waamini!

7 Kwa kweli, tayari mme-shindwa mnapokuwa na ma-shtaka ya kisheria wenyewe kwa wenyewe. Je, si afadhali mkubali kukosewa?^g Je, si afadhali mkubali kupunjwa? **8** Badala yake, mnawakosea na kuwapunja, tena ndugu zenu!

9 Au je, hamjui kwamba watu wasio waadilifu hawataurithi Ufalme wa Mungu?^h

SURA YA 5

a Mhu 12:14

b Mwa 3:23, 24
Kum 17:7
Tit 3:10
2Yo 10

SURA YA 6

c Mt 18:15-17

d Ufu 2:26, 27
Ufu 20:4

e Ro 16:20

f Mt 18:17

g Mt 5:39, 40

h Efe 5:5
Ufu 22:15

Safu ya 2

a Ufu 21:8

b Kol 3:5

c Ebr 13:4

d Ro 1:27
1Ti 1:9, 10

e 1Ko 5:11

f Kum 21:20, 21
Met 23:20
1Pe 4:3

g Ebr 12:14

h Mdo 22:16
Ebr 10:22i Efe 5:25, 26
2Th 2:13

j Ro 5:18

k 1Ko 10:23

l Ro 14:17

m 1Th 4:3

n Mdo 2:24

o 2Ko 4:14

p Ro 8:11
Efe 1:19, 20q Ro 12:4, 5
1Ko 12:18, 27
Efe 4:15
Efe 5:29, 30r Mwa 2:24
Mt 19:4, 5

Msipotoshwe.* Waasherati,^{#a} waabudu-sanamu,^b wazinzi,^c wanaume wanaofanya ngono na wanaume,^{△d} **10** wezi, watu wenye pupa,^e walevi,^f watakanaji,* na wanyang'anyi hawataurithi Ufalme wa Mungu.^g **11** Na bado baadhi yenu mlikuwa hivyo. Lakini mmeoshwa mkawa safi;^h mmetakaswa;ⁱ mmetangazwa kuwa waadilifu^j katika jina la Bwana Yesu Kristo na kwa roho ya Mungu wetu.

12 Mambo yote ni halali* kwangu, lakini si mambo yote yenye faida.^k Mambo yote ni halali kwangu, lakini sitaruhusu kitu chochote kinitawale.[#] **13** Chakula ni kwa ajili ya tumbo, na tumbo ni kwa ajili ya chakula, lakini Mungu atavifanya vyote viwe si kitu.^l Mwili si kwa ajili ya uasherati,* bali ni kwa ajili ya Bwana,^m na Bwana ni kwa ajili ya mwili. **14** Lakini Mungu alimfufua Bwanaⁿ na pia atafufua sisi kutoka kwenye kifo^o kupitia nguvu zake.^p

15 Je, hamjui kwamba mii-li yenu ni viungu vya Kristo?^q Basi, je, nivichukue viungu vya Kristo na kuviunganisha na kahaba? La hasha! **16** Je, hamjui kwamba yeyote ambaye ameungana na kahaba ni mwili mmoja naye? Kwa maana yeye anasema, “hao wawili watakuwa mwili mmoja.”^r

6:9 *Au “Msidanganywe.” #Angalia Kamusi, uku. 2012, “Uasherati.” △Au “wanaume wanaotenda au kukubali kutendewa mambo hayo.” Tnn., “wanaume wanaolala na wanaume.” **6:10** *Au “watu wanaotumia maneno machafu.” **6:12** *Au “yanakubalika.” #Au “sitakubali kuwa chini ya mamlaka ya kitu chochote.” **6:13** *Neno la Kigiriki, *por-nei*^a. Angalia Kamusi, uku. 2012.

17 Lakini yeyote anayeungana na Bwana ana umoja naye katika roho.^a **18** Ukimbieni uasherati!^{*b} Dhambi nyingine yoyote ambayo huenda mtu akafanya iko nje ya mwili wake, lakini yeyote aliye na mazoea ya kufanya uasherati anautendea dhambi mwili wake mwenyewe.^c **19** Je, hamjui kwamba mwili wenu ni hekalu^d la roho takatifu ndani yenu, mliyopokea kutoka kwa Mungu?^e Pia, ninyi si mali yenu wenyewe,^f **20** kwa maana mlinunuliwa kwa bei.^g Kwa vyovyote, mtukuzeni Mungu^h katika mwili wenu.ⁱ

7 Basi kuhusu mambo ambayo mliandika, ni bora mwanamume asinguse* mwanamke; **2** lakini kwa sababu ya kuenea kwa uasherati,* kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe^j na kila mwanamke awe na mume wake mwenyewe.^k **3** Mume na ampe mke wake haki yake, na mke pia na amfanyie vivyo hivyo mume wake.^l **4** Mke hana mamlaka juu ya mwili wake mwenyewe, bali mume wake anayo; vivyo hivyo, mume hana mamlaka juu ya mwili wake mwenyewe, bali mke wake anayo. **5** Msiwe mkinyimana ila kwa makubaliano kwa wakati uliowe kwa, ili mtenge wakati kwa ajili ya sala na mje pamoja tena, ili Shetani asiendeleo kuwajaribu kwa sababu mnakosa kujizuia.* **6** Hata hivyo, ninasema hilo ili kuwapa ruhusa, bali

6:18 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 7:1 *Yaani, asifanye ngono na. 7:2 *Neno la Kigiriki *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 7:5, 9 *Au "kujidhibiti; kujiweza."

SURA YA 6

a Yoh 17:20, 21

b Mwa 39:10-12
1Th 4:3

c Ro 1:24, 27

d 2Ko 6:16

e 1Ko 3:16

f Ro 14:8

g 1Ko 7:23
Ebr 9:12
1Pe 1:18, 19

h Mt 5:16

i Ro 12:1

SURA YA 7

j Met 5:18, 19

k Mwa 2:24
Ebr 13:4l Kut 21:10
1Ko 7:5

Safu ya 2

a Mt 19:10, 11

b 1Ko 7:39, 40
1Ko 9:5c 1Th 4:4, 5
1Ti 5:11, 14d Mt 5:32
Mt 19:6e Mk 10:11
Lu 16:18

f 1Ko 7:25, 40

g Ebr 12:14

h 1Pe 3:1, 2

si amri. **7** Lakini ningependa watu wote wawe kama mimi nilivyo. Hata hivyo, kila mmoja ana zawadi yake^a mwenyewe kutoka kwa Mungu, mmoja kwa njia hii, mwingine kwa njia ile.

8 Sasa ninawaambia waseja na wajane, ni bora wabaki kama mimi nilivyo.^b **9** Lakini ikiwa hawawezi kujizuia,* acheni wafunge ndoa, kwa maana ni bora kufunga ndoa kuliko kuwaka tamaa.^c

10 Kwa watu waliofunga ndoa ninatoa maagizo, si mimi bali ni Bwana, kwamba mke hapaswi kutengana na mume wake.^d **11** Lakini wakitengana, abaki bila kuolewa la sivyo apatane tena na mume wake; na mume hapaswi kumwacha mke wake.^e

12 Lakini kwa wale wengi-
ne ninawaambia, ndiyo, mimi, si Bwana:^f Ikiwa ndugu yeyote ana mke asiyeamini na mke huyo anakubali kuishi pamoja naye, basi asimwache; **13** na ikiwa mwanamke ana mume asiyeamini na mume huyo anakubali kuishi pamoja naye, basi asimwache mume wake. **14** Kwa maana mume asiyeamini hutakaswa kuhisiana na mke wake, na mke asiyeamini hutakaswa kuhisiana na huyo ndugu; la sivyo, watoto wenu hawangukuwa safi, lakini sasa wao ni watakatifu. **15** Lakini yule asiyeamini akiamua kuondoka,* acha aondoke; ndugu au dada hajafungwa chini ya hali kama hizo, lakini Mungu amewaita ninyi kwenye amani.^g **16** Wewe mke, unajuaje kama utamwokoa mume wako?^h Au

7:15 *Au "kutengana."

wewe mume, unajuaje kama utamwoko mke wako?

17 Hata hivyo, kama Yehova* alivyompa kila mmoja fungu, kila mmoja na ajiendeshe kama Mungu alivyomwita.^a Ninatoa agizo hilo katika makutaniko yote. **18** Je, mtu yeyote aliitwa akiwa tayari ametahiriwa?^b Basi asibadili kutahiriwa kwake. Je, mtu yeyote ameitwa akiwa hajatahiriwa? Basi asitahiriwe.^c **19** Kutahiriwa hakuna maana, wala kutotahiriwa hakuna maana;^d lakini kushika amri za Mungu kuna maana.^e **20** Basi katika hali yoyote ambayo kila mmoja aliitwa, acheni abaki hivyo.^f **21** Je, uliitwa ukiwa mtumwa? Usiache hilo likuhangaishe;^g lakini ikiwa unaweza kuwa huru, basi tumia nafasi hiyo. **22** Kwa maana yeyote aliyelitwa katika Bwana akiwa mtumwa ni mtu aliyelekwa huru wa Bwana;^h vivyo hivyo yeyote aliyelitwa akiwa mtu aliye huru ni mtumwa wa Kristo. **23** Mlinunuliwa kwa bei;ⁱ acheni kuwa watumwa wa wanadamu. **24** Akina ndugu, katika hali yoyote ambayo kila mmoja aliitwa, acheni abaki hivyo mbele za Mungu.

25 Sasa kuhusu mabikira,* sina amri kutoka kwa Bwana, lakini ninatoa maoni yangu nikiwa mtu aliyeonyeshwa rehema na Bwana kuwa waminifu. **26** Kwa hiyo, ninana ni bora kwa mtu kuendelea kama alivyo kwa sababu ya ugumu uliopo. **27** Je, umefungwa kwa mke? Acha kuta-

7:17 *Angalia Nyongeza A5. 7:25 *Au "wale ambao hawajawahi kufunga ndoa."

SURA YA 7

a 1Ko 7:7

b Mdo 21:20

c Mdo 10:45
Mdo 15:1, 24
Gal 5:2d Gal 6:15
Kol 3:11e Mhu 12:13
Yer 7:23
Ro 2:25
Gal 5:6
1Yo 5:3

f 1Ko 7:17

g Gal 3:28

h Yoh 8:36
Flm 15, 16i 1Ko 6:19, 20
Ebr 9:12
1Pe 1:18, 19j 1Ko 7:12
1Ko 7:40

Safu ya 2

a Mal 2:16
Mt 19:6
Efe 5:33b Ro 13:11
1Pe 4:7

c 1Ti 5:8

d 1Ti 5:5

futa kufunguliwa.^a Je, umewe kwa huru kutoka kwa mke? Acha kutafuta mke. **28** Lakini hata kama ukifunga ndoa, hutakuwa ukifanya dhambi. Na kama bikira akifunga ndoa, mtu huyo hatakuwa akifanya dhambi. Hata hivyo, wale wanaofanya hivyo watakuwa na dhiki katika mwili wao. Lakini ninajaribu kuwaepusha ninyi.

29 Isitoshe, ninasema hivi akina ndugu, wakati uliobaki umepungua.^b Tangu sasa wale walio na wake na wawe kana kwamba hawana, **30** na wale wanaolia wawe kama wale wasiolia, na wale wanaoshangilia wawe kama wale wasioshangilia, na wale wanaonunua wawe kama wale wasio na kitu, **31** na wale wanaoutumia ulimwengu wawe kama wale wasioutumia kwa ukamili; kwa maana tamasha ya ulimwengu huu inabadilika. **32** Kwa kweli, ninataka msihangaika. Mwanamume ambaye hajaoa huhangaikia mambo ya Bwana, jinsi anavyoweza kupata kibali cha* Bwana. **33** Lakini mwanamume aliyeo huhangaikia mambo ya ulimwengu,^c jinsi anavyoweza kupata kibali cha* mke wake, **34** naye amegawanyika. Zaidi ya hayo, mwanamke ambaye hajaolewa, na vilevile bikira, huhangaikia mambo ya Bwana,^d ili awe mtaakatifu katika mwili wake na pia katika roho yake. Hata hivyo, mwanamke aliyeo huhangaikia mambo ya ulimwengu, jinsi anavyoweza kupata kibali cha* mume wake. **35** Lakini ninasema hivyo kwa faida

7:32-34 *Au "kumpendeza."

yenu wenyewe, si ili niwazuie,* bali niwachochee kufanya jambo linalofaa na kumtumikia Bwana daima bila kukengeushwa fikira.

36 Lakini kama yeyote akiona kwamba anajiendesha isivyofaa kwa kubaki mseja,* na ikiwa amepita upeo wa ujana, basi inapaswa kuwa hivi: Acheni afanye anavyotaka; hafanyi dhambi. Acheni afunge ndoa.^a **37** Hata hivyo ikiwa yeyote ametulia moyoni mwake, na hana uhitaji wowote, lakini ana mamlaka juu ya nia yake mwenyewe naye amefanya uamuzi moyoni mwake kubaki mseja,* atafanya vema.^b **38** Vivyo hivyo yeyote anayefunga ndoa* anafanya vema, lakini yeyote asiyefunga ndoa atafanya vema zaidi.^c

39 Mke amefungwa kwa muda wote ambao mume wake yuko hai.^d Lakini mume wake akilala usingizi katika kifo, yuko huru kuolewa na yeyote anayemtaka, katika Bwana tu.^e **40** Lakini kwa maoni yangu, mwanamke huyo atakuwa na furaha zaidi akibaki kama alivyo; na ninafikiri mimi pia nina roho ya Mungu.

8 Basi kuhusu chakula kilichotolewa kwa sanamu:^f Tunajua sote tuna ujuzi.^g Ujuzi huleta majivuno, lakini upe-ndo hujenga.^h **2** Yeyote aki-fikiri anajua jambo fulani, bado hajalijua kama anavyo-paswa kulijua. **3** Lakini ikiwa yeyote anampenda Mungu, huyo anajulikana naye.

7:35 *Tnn., "nisiwawekee mtego." 7:36 *Au "kuelekea ubikira wake." 7:37 *Au "kuendelea kuwa bikira." 7:38 *Au "anayetoa ubikira wake katika ndoa."

SURA YA 7

a Mt 19:12
1Ko 7:28

b Mt 19:10, 11

c 1Ko 7:32

d Ro 7:2

e Mwa 24:2, 3
Kum 7:3, 4
Ne 13:25, 26
2Ko 6:14

SURA YA 8

f Mdo 15:20, 29

g Ro 14:14
1Ko 8:10

h 1Ko 8:13
1Ko 13:4, 5

Safu ya 2

a Kum 32:21
2Fa 19:17, 18
Yer 16:20

b Kum 6:4
Kum 32:39

c Zb 82:1, 6
Yoh 10:34, 35

d 1Ti 2:5

e Mal 2:10
Mt 23:9

f Mdo 17:28
Ro 11:36

g Yoh 1:1, 3
Kol 1:15, 16

h Ro 14:14

i 1Ko 10:27, 28

j Ro 14:23

k Ro 14:17

l Ebr 13:9

m Ro 14:13, 20

n Ro 14:15

1 WAKORINTHO 7:36-8:12

4 Sasa kuhusu kula chakula kilichotolewa kwa sanamu, tunajua kwamba sanamu si kitu^a ulimwenguni na kwamba hakuna Mungu isipokuwa mmoja.^b **5** Kwa maana hata ingawa kuna wale wanaoitwa miungu, iwe ni mbinguni au duniani,^c kama vile kulivyo na "miungu" mingi na "mabwana" wengi, **6** kwa kweli kwetu kuna Mungu mmoja^d aliye Baba,^e ambaye vitu vyote vimetoka kwake na sisi kwa ajili yake;^f na kuna Bwana mmoja, Yesu Kristo, ambaye vitu vyote vimepitia kwake^g na sisi kupitia kwake.

7 Hata hivyo, si watu wote walio na ujuzi huu.^h Lakini wengine, kwa sababu zamani waliabudu sanamu, wanakula chakula kama kitu kilichotolewa dhabihu kwa sanamu,ⁱ na dhamiri yao, kwa kuwa ni dhaifu, inatiwa unajisi.^j **8** Lakini chakula hakitafanya tumkaribie zaidi Mungu;^k hatupotezi chochote tusipokula, wala hatuongezi chochote tunapokula.^l **9** Lakini endeeleni kujihadhari kwamba haki yenu ya kuchagua isije ikawa kwa njia fulani kikwazo kwa wale walio dhaifu.^m **10** Kwa maana yeyote akikuona wewe uliye na ujuzi ukila mlo katika hekalu la sanamu, je, dhamiri ya huyo aliye dhaifu hai- tapata ujasiri kufikia hatua ya kula chakula kilichotolewa kwa sanamu? **11** Basi, kwa ujuzi wako, mtu ambaye ni dhaifu anaharibiwa, ndugu yako ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake.ⁿ **12** Mnapo- watendea dhambi ndugu zenu katika njia hii na kuiumiza

dhamiri yao dhaifu,^a mnamtendea dhambi Kristo. **13** Kwa sababu hiyo, ikiwa chakula kinamkwaza ndugu yangu, mimi sitakula nyama tena kamwe, ili nisije nikamkwaza ndugu yangu.^b

9 Je, mimi siko huru? Je, mimi si mtume? Je, mimi sijamwona Yesu Bwana wetu?^c Je, ninyi si kazi yangu katika Bwana? **2** Hata kama mimi si mtume kwa wengine, hakika mimi ni mtume kwenu! Kwa maana ninyi ndio muhuri unaothibitisha utume wangu katika Bwana.

3 Kwa wale wanaonichunguza, ninajitetea hivi: **4** Sisi tuna haki* ya kula na kunywa, sivyo? **5** Sisi tuna haki ya kuambatana na mke ambaye ni mwamini,^{*d} kama wale mitume wengine na ndugu za Bwana^e na Kefa,^{#f} sivyo? **6** Au je, ni Barnaba^g na mimi pekee ambao hatuna haki ya kupata riziki bila kufanya kazi? **7** Ni mwanajeshi gani ambaye hutumika kwa gharama yake mwenyewe? Ni nani anayepanda shamba la mizabibu naye asile matunda yake?^h Au ni nani anayechunga mifugo naye asinywe maziwa ya mifugo yake?

8 Je, ninasema mambo haya kwa maoni ya kibinadamu? Au je, Sheria haisemi mambo hayo pia? **9** Kwa maana imeandikwa katika Sheria ya Musa: “Hupaswi kumfunga kinywa ng’ombe dume anapopura nafaka.”ⁱ Je, ng’ombe dume ndio Mungu anaohangaikia? **10** Au,

9:4, 12 *Tnn., “mamlaka.” 9:5 *Au “kuwa na dada akiwa mke.” #Pia anaitwa Petro.

SURA YA 8

a 1Ko 10:28, 29

b Mt 18:6
Ro 14:15, 21

SURA YA 9

c Mdo 9:3-5
1Ko 15:7, 8

d Mt 19:11

e Mt 13:55
Gal 1:19

f Yoh 1:42

g Mdo 13:2

h Kum 20:6
Met 27:18i Kum 25:4
1Ti 5:18

Safu ya 2

a Ro 15:26, 27
Gal 6:6
Flp 4:15-17b Mdo 18:3
Mdo 20:34
2Th 3:7, 8c 2Ko 6:3
2Ko 11:7d Law 6:14, 16
Hes 18:30, 31
Kum 18:1e Mt 10:9, 10
Lu 10:7, 8f Mdo 18:3
Mdo 20:34
1Ko 4:11, 12
2Th 3:8

g 2Ko 11:8-10

h Eze 3:18

i Gal 2:7
Efe 3:1, 2
Kol 1:25

je, kweli anasema hivyo kwa ajili yetu? Kwa hakika hilo liliandikwa kwa ajili yetu, kwa sababu mtu anayelima na mtu anayepura anapaswa kufanya hivyo akiwa na tumaini la kupata fungu.

11 Ikiwa tumepanda vitu vya kiroho miongoni mwenu, je, ni jambo kubwa tukivuna kutoka kwenu vitu vya kimwili?^a **12** Ikiwa watu wengine wana haki ya kuwadai ninyi jambo hilo, je, sisi hatuna haki hiyo hata zaidi? Hata hivyo, hatujatumia haki* hii,^b bali tunavumilia mambo yote, ili kwa vyovyote tusiizuie habari njema kumhusu Kristo.^c **13** Je, hamjui kwamba watu wanaofanya kazi takatifu hula vitu vya hekalu, na kwamba wale wanaohudumu kwa kawaida kwenye madhabahu hupata fungu lao kutoka kwenye madhabahu?^d **14** Vivyo hivyo, pia, Bwana aliamuru kwamba wale wanaotangaza habari njema waishi kupitia habari njema.^e

15 Lakini kati ya mipango hiyo sijatumia hata mmoja.^f Kwa kweli, sijaandika mambo haya ili nifanyiwe jambo hilo, kwa maana ingekuwa bora kwangu kufa kuliko—hakuna mtu atakayeondoa sababu zangu za kujisifu!^g **16** Sasa ikiwa ninatangaza habari njema, hivyo si sababu ya kufanya nijisifu, kwa maana nimewekewa sharti. Kwa kweli, ole wangu nisipotangaza habari njema!^h **17** Nikifanya hivyo kwa kupeenda, nina thawabu; lakini hata nikifanya hivyo bila kupenda, bado nimekabidhiwa usimamizi.ⁱ **18** Basi, thawabu yangu ni nini? Kwamba ninapo-

tangaza habari njema, niitoe habari njema bila gharama, ili nisitumie vibaya mamlaka* yangu katika habari njema.

19 Kwa maana, ingawa niko huru kutoka kwa watu wote, nimejifanya kuwa mtumwa kwa wote, ili niwapate watu wengi iwezekanavyo. **20** Kwa Wayahudi nilikuwa kama Myahudi, ili niwapate Wayahudi;^a kwa wale walio chini ya sheria nilikuwa kama aliye chini ya sheria, ingawa mimi mwenyewe siko chini ya sheria, ili niwapate wale walio chini ya sheria.^b **21** Kwa wale wasio na sheria nilikuwa kama asiye na sheria, ingawa mimi siko bila sheria kwa Mungu bali niko chini ya sheria kwa Kristo,^c ili niwapate wale wasio na sheria. **22** Kwa walio dhafu nilikuwa dhafu, ili niwapate walio dhafu.^d Nimekuwa mambo yote kwa watu wa namna zote, ili kwa vyovyote niwaokoe wengine. **23** Lakini ninafanya mambo yote kwa ajili ya habari njema, ili niishiriki pamoja na wengine.^e

24 Je, hamjui kwamba wakimbiaji wote katika mbio hukimbia, lakini ni mmoja tu anayepokea tuzo? Kimbieni kwa njia itakayowawezesha kushinda tuzo.^f **25** Sasa kila mtu anayeshiriki katika shindano* hujizuia^g katika mambo yote. Bila shaka, wao hushindana ili wapate taji linaloweza kuharibika,^g lakini sisi taji lisiloharibika.^h **26** Kwa hiyo, jinsi ninavyokimbia si bila kusudi;ⁱ jinsi ninavyoelekeza ngumi zangu ni ili nisiwe nikipiga hewa; **27** lakini ni-

9:18 *Au "haki." 9:25 *Au "kila mwariadha." #Au "hujidhibiti."

SURA YA 9

a Mdo 16:3
Mdo 18:18

b Mdo 21:24, 26

c Yoh 13:34
Gal 6:2

d Ro 14:1
Ro 15:1
ZKo 11:29

e Mdo 19:26
1Th 2:8

f Mt 10:22
Flp 3:14
2Ti 4:7, 8

g 2Ti 2:5

h Yak 1:12

i Gal 2:2
Flp 2:16
Ebr 12:1

Safu ya 2

a Ro 8:13
Kol 3:5

SURA YA 10

b Kut 13:21

c Kut 14:21, 22

d Kut 16:14, 15

e Kut 17:6

f Hes 20:11
Yoh 4:10, 25

g Hes 14:29
Hes 14:35

h Hes 11:4, 34

i Kut 32:4, 6

j Hes 25:1, 9

k Kum 6:16

l Hes 21:5, 6
Mt 4:7

m Hes 14:2

n Hes 14:36, 37

naupigapiga* mwili wangu^a na kuuongoza kama mtumwa, ili baada ya kuwahubiria wengine, kwa njia fulani mimi mwenyewe nisikataliwe.[#]

10 Basi akina ndugu, nina-taka mjue kwamba mababu zetu wote walikuwa chini ya wingu^b na wote walipita katika bahari^c **2** na wote walibatizwa katika Musa kupitia wingu na bahari, **3** na wote walikula chakula kilekile cha kiroho^d **4** na wote walikunywa maji yaleyale ya kiroho.^e Kwa maana walikuwa wakinywa kutokana na mwamba wa kiroho uliowafuata, na mwamba huo ulimaanisha* Kristo.^f **5** Hata hivyo, Mungu hakupendezwa na wengi wao, kwa maana waliangamizwa nyikani.^g

6 Basi mambo hayo yalikuwa vielelezo kwetu, ili tusitamani mambo mabaya, kama wao walivyotamani.^h **7** Wala tusiwe waabudu sanamu, kama baadhi yao walivyofanya; kama ilivyoandikwa: "Watu wakaketi ili wale na kunywa. Kisha wakasimama ili wajitumbuize."ⁱ **8** Wala tusifanye uasherati,* kama baadhi yao walivyofanya uasherati,* na 23,000 kati yao wakaanguka kwa siku moja.^j **9** Wala tusimjaribu Yehova,*^k kama baadhi yao walivyomjaribu, wakaangamizwa na nyoka.^l **10** Wala tusiwe wanung'unikaji,^m kama baadhi yao walivyonung'unika, wakaangamizwa na mwangamizaji.ⁿ

9:27 *Au "ninauadhibu; ninautia nidhamu sana." #Au "nikose kustahili." 10:4 *Au "ulikwa." 10:8 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 10:9 *Angalia Nyo-ngeza A5.

11 Basi mambo hayo yaliwapa ili kuwa vielelezo, nayo yaliandikwa ili kuwa onyo kwetu sisi^a ambao tumefikiwa na miisho ya mifumo ya mambo.

12 Basi yule anayefikiri amesimama na ajihadhari asije akaanguka.^b **13** Hakuna majaribu ambayo yamewapata ninyi ila yale yaliyo ya kawaida kwa watu.^c Lakini Mungu ni mwaminifu, naye hatawaacha mjaribiwe kupita mnavyoweza kuhimili,^d bali pamoja na majaribu hayo atafanya pia njia ya kutokea ili mweze kuyavumilia.^e

14 Kwa hiyo, wapendwa wangu, ikimbieni ibada ya sanamu.^f **15** Ninasema kana kwamba ni kwa watu wenye utambuzi; hukumuni wenyewe lile ninalosema. **16** Kikombe cha baraka ambacho tunabariki, je, si kushiriki katika damu ya Kristo?^g Mkate ambao tunamega, je, si kushiriki katika mwili wa Kristo?^h **17** Kwa sababu kuna mkate mmoja, sisi, ingawa tuko wengi, ni mwili mmoja,ⁱ kwa maana sote tunakula mkate huo mmoja.

18 Tazameni Israeli kwa njia ya kimwili: Je, wale wanaokula dhabihu si washiriki pamoja na madhabahu?^j **19** Basi, niseme nini? Je, kile kilichotolewa dhabihu kwa sanamu ni kitu, au je, sanamu ni kitu? **20** Hapana; bali ninasema kwamba vitu ambavyo mataifa huvitoa dhabihu, wao huvitoa dhabihu kwa roho waovu, si kwa Mungu;^k nami sitaki muwe washiriki pamoja na roho waovu.^l **21** Hamwezi kuwa mki-

SURA YA 10

a Ro 15:4

b Met 28:14
Lu 22:33, 34
Gal 6:1

c 1Pe 5:8, 9

d Lu 22:31, 32
2Pe 2:9e Isa 40:29
Flp 4:13f Kum 4:25, 26
2Ko 6:17
1Yo 5:21

g Mt 26:27, 28

h Mt 26:26
Lu 22:19
1Ko 12:18

i Ro 12:5

j Law 7:15

k Kum 32:17

l Yud 6

Safu ya 2

a Eze 41:22
Mal 1:12b Kut 34:14
Kum 32:21c Ro 14:19
Ro 15:2d 1Ko 10:32, 33
1Ko 13:4, 5
Flp 2:4e Zb 24:1
1Ti 4:4

f 1Ko 8:7, 10

g Ro 14:15, 16
1Ko 8:12h Ro 14:6
1Ti 4:3i Mt 5:16
Kol 3:17

nywa kikombe cha Yehova* na kikombe cha roho waovu; hamwezi kuwa mkishiriki “meza ya Yehova”^{**a} na meza ya roho waovu. **22** Au je, ‘tunamchochea Yehova* kuwa na wivu’?^b Je, sisi tuna nguvu zaidi kuliko yeye?

23 Mambo yote ni halali,* lakini si mambo yote yaliyo na faida. Mambo yote ni halali, lakini si mambo yote yanayojenga.^c **24** Kila mmoja na aendelee kutafuta, si faida yake mwenyewe, bali faida ya yule mtu mwingine.^d

25 Kuleni chochote kinachouzwa katika soko la nyama, bila kuchunguza kwa sababu ya dhamiri yenu, **26** kwa maana “dunia na vyote vilivyomo ni vya Yehova.”^{**e}

27 Mtu asiyeamini akiwaalika nanyi mtake kwenda, kuleni chochote kinachowekwa mbele yenu, bila kuchunguza kwa sababu ya dhamiri yenu.

28 Lakini yeyote akiwaambia, “Hiki ni kitu kilichotolewa katika dhabihu,” msile kwa sababu ya yule aliyewaambia na kwa sababu ya dhamiri.^f

29 Simaanishi dhamiri yako mwenyewe, bali ya yule mtu mwingine. Kwa maana kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine?^g

30 Ikiwa ninakula nikiwa na shukrani, kwa nini nitukanwe juu ya kile ninachotolea shukrani?^h

31 Kwa hiyo, iwe mnakula au mnakunywa au mnafanya jambo lingine lolote, fanyeni mambo yote kwa utukufu wa Mungu.ⁱ **32** Epukeni kuwa vikwazo kwa Wayahudi

10:21, 22, 26 *Angalia Nyongeza A5.
10:23 *Au “yanakubalika.”

na vilevile kwa Wagiriki na kwa kutaniko la Mungu,^a **33** kama vile ninavyojaribu kuwapendeza watu wote katika mambo yote, bila kutafuta faida yangu mwenyewe,^b bali faida ya walio wengi, ili wapate kuokolewa.^c

11 Iweni waigaji wangu, kama vile mimi nilivyo mwigaji wa Kristo.^d

2 Ninawapongeza kwa sababu katika mambo yote mnanikumbuka na mnayashika mapokeo kama vile nilivyowapa. **3** Lakini ninataka mjue kwamba kichwa cha kila mwanamume ni Kristo;^e nacho kichwa cha mwanamke ni mwanamume;^f nacho kichwa cha Kristo ni Mungu.^g **4** Kila mwanamume ambaye husali au kutoa unabii akiwa na kitu juu ya kichwa chake hukiaibisha kichwa chake; **5** lakini kila mwanamke anayesali au kutoa unabii^h bila kufunika kichwa chake anakiaibisha kichwa chake, kwa maana ni kana kwamba yeye ni mwanamke mwenye kichwa kilichonyolewa. **6** Kwa maana ikiwa mwanamke hajifuniki, anapaswa kukatwa nywele zake; lakini ikiwa ni aibu kwa mwanamke kukatwa nywele au kunyolewa, anapaswa ajifunike.

7 Kwa maana mwanamume hapaswi kufunika kichwa chake, kwa kuwa yeye ni mfano na utukufu wa Mungu,ⁱ lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume. **8** Kwa maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke alitoka katika mwanamume.^j **9** Isitoshe, mwanamume ha kuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili

SURA YA 10

a Ro 14:13
1Ko 8:13
2Ko 6:3

b Ro 15:2
Flp 2:4

c 1Ko 9:22

SURA YA 11

d Flp 3:17
2Th 3:9

e Ro 14:9
Efe 4:15
Kol 2:10

f Efe 5:23
1Pe 3:1

g 1Ko 15:27, 28

h Yoe 2:28
Mdo 21:8, 9

i Mwa 1:27

j Mwa 2:22, 23

Safu ya 2

a Mwa 2:18

b 1Ko 4:9

c Mwa 2:21, 22

d 1Ko 8:6

e Mdo 20:29, 30
1Ko 1:12
1Ti 4:1
2Pe 2:1

f Lu 22:19, 20

ya mwanamume.^a **10** Ndiyo sababu mwanamke anapaswa kuwa na ishara ya mamlaka juu ya kichwa chake kwa sababu ya malaika.^b

11 Tena, kuhusiana na Bwana, mwanamke hajatengani-shwa na mwanamume wala mwanamume hajatenganishwa na mwanamke. **12** Kwa maana kama vile mwanamke alivyotoka katika mwanamume,^c vivyo hivyo pia mwanamume amepitia katika mwanamke; lakini vitu vyote vime-toka kwa Mungu.^d **13** Hukumu ni wenyewe: Je, inafaa mwanamke kusali kwa Mungu bila kufunika kichwa chake? **14** Je, maumbile yenyewe hayawafundishi kwamba nywele ndefu ni aibu kwa mwanamume, **15** lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu, ni utukufu kwake? Kwa maana amepewa nywele zake ziwe kitu cha kujifunika. **16** Hata hivyo, mtu yeyote akitaka kubishania desturi nyingine, sisi hatuna nyingine, wala makutaniko ya Mungu.

17 Lakini ninapoyatoa maa-gizo haya, siwapongezi ninyi, kwa sababu mnakutana pamoja, si kwa ajili ya wema, bali kwa ajili ya ubaya. **18** Kwanza kabisa, nasikia kwamba mnapokutana katika kutaniko, kuna migawanyiko kati yenu; na kwa kadiriri fulani ni-naamini jambo hilo. **19** Kwa maana lazima kutakuwa na madhehebu miongoni mwen-u,^e ili wale waliokubaliwa kati yenu waonekane.

20 Mnapokutana mahali pamoja, kwa kweli si kwa sababu ya kula Mlo wa Jioni wa Bwana.^f **21** Kwa maana mnapokula, kila mtu hutangulia kula

mlo wake mwenyewe wa jioni, hivi kwamba mmoja ana njaa lakini mwingine amelewa. **22** Je, hamna nyumba ambamo mnaweza kula na kunywa? Au je, mnalidharau kutaniko la Mungu na kuwaaibisha wale wasio na kitu? Niwaambie nini ninyi? Je, niwapongeze? Kuhusu hilo siwapongezi.

23 Kwa maana nilipokea kutoka kwa Bwana kile nilichowapa ninyi pia, kwamba Bwana Yesu katika usiku^a ambao alisalitiwa alichukua mkate, **24** na baada ya kutoa shukrani, akaumega na kusema: "Huu unamaanisha mwili wangu,^b ambao ni kwa ajili yenu. Endeleeni kufanya hivi kwa kunikumbuka."^c **25** Akafanya vivyo hivyo na kile kikombe^d pia, baada ya wao kula mlo wa jioni, akisema: "Kikombe hiki kinamaanisha agano^e jipya kwa msingi wa damu yangu.^f Endeleeni kufanya hivi, kila mara mnapokinywa, kwa kunikumbuka mimi."^g **26** Kwa maana kila mara mnapokula mkate huu na kunywa kikombe hiki, mnaendelea kukitangaza kifo cha Bwana, mpaka atakapokuja.

27 Kwa hiyo, yeyote anayekula mkate au kukinywa kikombe cha Bwana isivyofaa atakuwa na hatia kuhusiana na mwili na damu ya Bwana. **28** Kwanza, acheni mtu ajichunguze mwenyewe na kuona kama anafaa,^h ndipo ale mkate na anywe kikombe. **29** Kwa maana yule anayekula na kunywa bila kuutambua mwili, anakula na kunywa hukumu dhidi yake mwenyewe. **30** Ndiyo sababu wengi

SURA YA 11

a Mt 26:20
Lu 22:14

b Mt 26:26
Mk 14:22
Ro 7:4
1Ko 10:17

c Lu 22:19

d Mt 26:27
Mk 14:23
1Ko 10:16

e Yer 31:31
Ebr 8:8
Ebr 9:15

f Lu 22:20
Ebr 9:13,14
1Pe 1:18,19

g Kut 12:14

h 2Ko 13:5

Safu ya 2

a 1Th 5:6

b Ebr 12:5

c 2Pe 2:20
2Pe 3:7

d 1Ko 11:29

SURA YA 12

e 1Ko 14:1

f Zb 115:5
Hab 2:18
1Ko 8:4
Gal 4:8
1Th 1:9

g 1Yo 4:2,3

h Efe 4:4

i Efe 4:11

j 1Pe 4:11

k 1Ko 14:26

kati yenu ni dhaifu na wagnjwa, na wengi wamelala usingizi katika kifo.^{*a} **31** Lakini kama tungetambua jinsi sisi wenyewe tulivyo, hatungehukumiwa. **32** Hata hivyo, tunapohukumiwa, Yehova^{*b} anatutia nidhamu, ili tusihukumiwe pamoja na ulimwengu.^c **33** Kwa hiyo, ndugu zangu, mnapokutana pamoja ili kula mlo huo, mngojeane. **34** Ikiwa yeyote ana njaa, acheni ale nyumbani, ili mnapokutana pamoja isiwe kwa ajili ya kuhukumiwa.^d Lakini kuhusu mambo waliyobaki, nitayarekebisha nitakapofika.

12 Basi kuhusu zawadi za kiroho,^e akina ndugu, sitaki mkose kujua. **2** Mnajua kwamba mlipokuwa watu wa mataifa,^{*} mliukuwa mkishawishiwa na kuziabudu sanamu zisizo na sauti,^f mki-zifuata popote zilipowaongoza. **3** Sasa ningetaka mjue kwamba hakuna mtu yeyote ambaye anaposema kwa roho ya Mungu, husema: "Yesu amelaaniwa!" na hakuna mtu anayeweza kusema: "Yesu ni Bwana!" isipokuwa kwa roho takatifu.^g

4 Basi kuna zawadi mbalimbali, lakini kuna roho ileile;^h **5** na kuna huduma mbalimbali,ⁱ na bado kuna Bwana yuleyule; **6** na kuna utendaji^{*} mbalimbali, na bado ni Mungu yuleyule anayefanya utendaji huo wote katika kila mtu.^j **7** Lakini roho hufunuliwa katika kila mmoja kwa kusudi lenye faida.^k **8** Kwa maana mtu mmoja

11:30 *Inaonekana inamaanisha kifo cha kiroho. **11:32** *Angalia Nyongeza A5. **12:2** *Yaani, watu wasio waamini. **12:6** *Au "kazi."

hupewa maneno ya* hekima kupitia roho, mwingine maneno ya ujuzi kulingana na roho ileile, **9** mwingine imani^a kwa roho ileile, mwingine zawadi za uponyaji^b kwa roho hiyo moja, **10** naye mwingine hupewa utendaji wa mateendo yenye nguvu,^c mwingine kutoa unabii, mwingine utambuzi wa maneno yaliyoongozwa na roho,^d mwingine lugha* mbalimbali,^e na mwingine fasiri ya lugha.^f **11** Lakini ni roho ileile inayofanya utendaji huu wote, ikimgawia kila mmoja kama vile inavyopenda.

12 Kwa maana kama vile mwili ni mmoja lakini una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili huo, ingawa ni vingi, ni mwili mmoja,^g ndivyo pia alivyo Kristo. **13** Kwa maana kwa roho moja sote tulibatiwa katika mwili mmoja, iwe ni Wayahudi au ni Wagiriki, iwe ni watumwa au ni walio huru, nasi sote tulinyewesha roho moja.

14 Kwa maana kwa kweli, mwili una viungo vingi, si kiungo kimoja.^h **15** Ikiwa mguu ungesema, "Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si sehemu ya mwili," hilo halifanyi usiwe sehemu ya mwili. **16** Na ikiwa sikio lingesema, "Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si sehemu ya mwili," hilo halilifanyi lisiwe sehemu ya mwili. **17** Ikiwa mwili wote ungekuwa jicho, kusikia kungekuwa wapi? Ikiwa wote ungekuwa sikio, kunusa kungekuwa wapi? **18** Lakini sasa Mungu amepanga kila kiungo cha mwili kama alivyopenda.

12:8 *Au "ujumbe wa." 12:10 *Au "ndimi."

SURA YA 12

a 1Ko 13:2

b Mdo 3:5-8
Mdo 28:8, 9

c Ebr 2:3, 4

d 1Yo 4:1

e Mdo 10:45, 46
1Ko 14:18

f 1Ko 14:26

g Ro 12:4, 5

h Efe 4:16

Safu ya 2

a Mwa 3:7, 21

b Ro 12:10
Gal 6:2
Efe 4:25

c Ebr 13:3

d Ro 12:15

e Efe 1:22, 23

f Ro 12:4, 5

g Efe 2:20

h Mdo 13:1

i Efe 4:11

j Gal 3:5

k Mdo 5:16

l Ebr 13:17

m Mdo 2:6, 7

19 Ikiwa vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? **20** Lakini sasa viungo ni vingi, lakini mwili mmoja. **21** Jicho haliwezi kuuambia mkono, "Sikuhitaji wewe," au tena kichwa haliwezi kuiambia miguu, "Siwahitaji ninyi." **22** Badala yake viungo vya mwili vinavyonekana kuwa dhaifu zaidi ni muhimu sana, **23** na sehemu za mwili ambazo tunafikiri hazistahili kuheshimiwa sana, tunazipa heshima zaidi,^a basi sehemu zetu ambazo hazivutii tunazitendea kwa heshima* zaidi, **24** bali sehemu zetu zinazopendeza hazihitaji kitu chochote. Lakini hivyo ndivyo Mungu alivyouunganisha mwili, akiipa heshima zaidi sehemu iliyokuwa na upungufu, **25** ili kusiwe na mgawanyiko katika mwili, bali viungo vyake vitunzane.^b **26** Kiungo kimoja kikiumia, viungo vingine vyote huumia pamoja nacho;^c au kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vingine vyote hushangilia pamoja nacho.^d

27 Basi ninyi ni mwili wa Kristo,^e na kila mmoja wenu ni kiungo cha mwili huo.^f

28 Naye Mungu amewaweka watu mbalimbali katika kutaniko: kwanza, mitume;^g pili, manabii;^h tatu, walimu;ⁱ kisha matendo yenye nguvu;^j kisha zawadi za uponyaji;^k huduma za kusaidia; uwezo wa kuelekeza;^l na lugha mbalimbali.^m **29** Je, wote ni mitume? Je, wote ni manabii? Je, wote ni walimu? Je, wote hufanya matendo yenye nguvu? **30** Je, wote wana zawadi za

12:23 *Au "kiasi."

uponyaji? Je, wote husema kwa lugha?^a Je, wote ni wakalimani?^{*b} **31** Lakini endeeleni kutafuta kwa bidii* zawadi zilizo kubwa zaidi.^c Na bado nitawaonyesha njia iliyo bora zaidi.^d

13 Nikisema kwa lugha za wanadamu na za malai-ka lakini sina upendo, nimekuwa chuma kinachovuma au toazi linalolia. **2** Na ikiwa nina zawadi ya kutoa unabii nami ninazielewa siri zote takatifu na ujuzi wote,^e na ikiwa nina imani yenye nguvu hata niweze kuhamisha* milima, lakini sina upendo, mimi si kitu.^{#f} **3** Nami nikitoa mali zangu zote ili kuwalisha wengine,^g na nikiutoa mwili wangu ili nijisifu, lakini sina upendo,^h sipati faida yoyote.

4 Upendoⁱ ni wenye subira*^j na fadhili.^k Upendo hauna wivu.^l Haujigambi, haujivuni,^m haujiendeshi bila adabu,ⁿ hautafuti faida zake wenyewe,^o hauchokozeki.^p Hauweki hesabu ya ubaya.*^q **6** Haulishangilii ukosefu wa uadilifu,^r bali hushangilia pamoja na kweli. **7** Huhimili mambo yote,^s huamini mambo yote,^t hutumaini mambo yote,^u huvumilia mambo yote.^v

8 Upendo haushindwi kamwe. Lakini kama kuna zawadi za unabii, zitaondolewa; kama kuna lugha,* zitakoma; kama kuna ujuzi, utaondolewa. **9** Kwa maana tuna ujuzi usio kamili^w nasi tunatoa unabii usio kamili; **10** lakini kile

12:30 *Au "watafsiri." 12:31; 14:1 *Au "kujitahidi kupata." 13:2 *Au "kusogeza." #Au "sifai kitu." 13:4 *Au "ustahimilivu." 13:5 *Au "makosa." 13:8 *Yaani, kuzungumza lugha nyingine ki-mujiza.

SURA YA 12

a 1Ko 14:4

b 1Ko 14:5

c 1Ko 14:1

d 1Ko 13:8

SURA YA 13

e 1Ko 12:8

f 1Yo 4:20

g Mt 6:2

h 2Ko 9:7

i 1Yo 4:8

j 1Th 5:14

k Ro 13:10

Efe 4:32

l Gal 5:26

m 1Pe 5:5

n Ro 13:13

1Ko 14:40

o 1Ko 10:24

Flp 2:4

p Mt 5:39

Yak 1:19

q Efe 4:32

Kol 3:13

r Ro 12:9

s 1Pe 4:8

t Mdo 17:11

u Ro 8:25

Ro 12:12

v 1Th 1:3

w Met 4:18

Safu ya 2

a Mt 22:37

Ro 13:10

SURA YA 14

b 1Th 5:20

c 1Ko 14:5

d 1Ko 13:2

e 1Ko 12:30

f Yoe 2:28

Mdo 2:17

Mdo 21:8, 9

kilicho kamili kitakapokuja, kile kisicho kamili kitaondolewa. **11** Nilipokuwa mtoto, nilikuwa nikisema kama mtoto, nikifikiri kama mtoto, nikiwaza kama mtoto; lakini kwa kuwa sasa nimekuwa mtu mzima, nimeziacha tabia za mtoto. **12** Kwa maana sasa tunaona kwa njia isiyo ya waziwazi* kupitia kioo cha chuma, lakini wakati huo itakuwa uso kwa uso. Kwa sasa sijui kikamili, lakini wakati huo nitajua kwa usahihi,[#] kama vile ninavyojulikana kwa usahihi. **13** Hata hivyo, sasa yanabaki mambo haya matatu: imani, tumaini, upendo; lakini lililo kubwa zaidi kati ya hayo ni upendo.^a

14 Fuatieni upendo, na bado endeeleni kutafuta kwa bidii* zawadi za kiroho, lakini ni afadhali zaidi kwamba mtoe unabii.^b

2 Kwa maana yule anayesema kwa lugha, hasemi na wanadamu, bali na Mungu, kwa maana hakuna anayeskiliza,^c bali yeye husema kwa roho siri zilizo takatifu.^d **3** Hata hivyo, yule anayetoa unabii huwajenga na kuwatia moyo na kuwafariji watu kwa maneno yake. **4** Yule anayesema kwa lugha hujijenga mwenyewe, lakini yule anayetoa unabii hulijenga kutaniko. **5** Basi ningependa ninyi nyote msemi kwa lugha,^e lakini ninapendelea zaidi mtoe unabii.^f Kwa kweli, yule anayetoa unabii ni mkubwa kuliko yule anayezungumza kwa lugha, isipokuwa afasiri* kwa ajili ya kutaniko ili lijengwe. **6** Lakini wakati

13:12 *Au "iliyo hafifu." #Au "kikamili." 14:5 *Au "atafsiri."

huu, akina ndugu, kama ningekuwa kwenu nikisema kwa lugha, ningewapa faida gani kama singezungumza nanyi kwa ufunuo^a au kwa ujuzi^b au kwa unabii au kwa fundisho?

7 Ndivyo ilivyo pia kwa vitu visivyo na uhai ambavyo hutoa sauti, iwe ni filimbi au kinubi. Kusipokuwa na tofauti kati ya sauti, kinachopigwa kwenye filimbi au kwenye kinubi kitajulikana-je? **8** Kwa maana tarumbeta ikipiga mwito usiojulikana, ni nani atakayejitayari-sha kwa ajili ya vita? **9** Vivyo hivyo, msiposema maneno yanayoeleweka kwa urahisi kupitia lugha hiyo, watu watajuaje kinachosemwa? Kwa kweli, mtakuwa mki-zungumza hewani. **10** Henda kuna aina nyingi za maneno ulimwenguni, hata hivyo hakuna aina isiyo na maana. **11** Ikiwa sielewi maana ya maneno, nitakuwa mgeni kwa yule anayezungumza, naye anayezungumza atakuwa mgeni kwangu. **12** Nanyi pia, kwa kuwa mnatamani sana zawadi za roho, jitahidini kujawa na zawadi ambazo zitalijenga kutaniko.^c

13 Kwa hiyo, yule anayezungumza kwa lugha na asali ili afasiri.^{*d} **14** Kwa maana ikiwa ninasali kwa lugha, ni zawadi yangu ya roho inayosali, lakini akili yangu haizai matunda. **15** Basi, nini kifanywe? Nitasali kwa zawadi ya roho, lakini nitasali pia kwa akili yangu. Nitaimba sifa kwa zawadi ya roho, lakini pia nitaimba sifa kwa akili ya-

14:13 *Au "atafasiri."

SURA YA 14

a Gal 1:11, 12
Gal 2:2

b 1Ko 12:8

c 1Ko 12:7
1Ko 14:4, 26

d 1Ko 12:8, 10
1Ko 14:5

Safu ya 2

a 1Ko 14:4

b Efe 4:14

c Ro 16:19

d Ebr 5:13, 14

e Isa 28:11, 12

f Mdo 2:4, 13

ngu. **16** Kama sivyo, ukitoa sifa kwa zawadi ya roho, mtu wa kawaida miongoni mweni atasemaje "Amina" unapotoa shukrani, kwa kuwa hajui unachosema? **17** Kweli, unatoa shukrani kwa njia nzuri, lakini yule mtu mwingine hajengwi. **18** Ninamshukuru Mungu kwamba ninasema kwa lugha nyingi kuliko ninyi nyote. **19** Hata hivyo, katika kutaniko afadhali nise-me maneno matano kwa akili yangu,^{*} ili pia niwafundishe[#] wengine, kuliko maneno elfu kumi kwa lugha.^a

20 Akina ndugu, msiiwe watoto wadogo katika uelewaji wenu,^b lakini iweni watoto wadogo kuhusiana na ubaya;^c nanyi muwe watu wazima katika uelewaji wenu.^d **21** Katika Sheria imeandikwa: "Nita-zungumza na watu hawa kwa lugha za watu wa kigeni na kwa midomo ya wageni, na hata wakati huo wata-kataa kunisikiliza,"^e asema Yehova.^{**e} **22** Kwa hiyo, lugha si ishara kwa ajili ya waamini bali kwa wasio waamini,^f lakini unabii si kwa ajili ya wasio waamini bali ni kwa ajili ya waamini. **23** Basi kutaniko lote likikusanyika mahali pamoja na wote waseme kwa lugha, nao watu wa kawaida au wasio waamini waingie, je, hawatasema kwamba ninyi mmerukwa na akili? **24** Lakini ikiwa nyote mnatoa unabii na mtu asiye mwamini au mtu wa kawaida aingie, atakaripiwa na kuchunguzwa na wote. **25** Siri za moyo wake

14:19 *Au "uelewaji." #Au "niwafundishe kwa mdomo." 14:21 *Angalia Nyo-ngeza A5.

zitakuwa wazi, hivi kwamba ataanguka kifudufudi na kumwabudu Mungu, akitangaza: "Kwa kweli Mungu yupo kati yenu."^a

26 Basi, tuseme nini akina ndugu? Mnapokusanyika pamoja, mmoja ana zaburi, mwingine ana fundisho, mwingine ana ufunuo, mwingine ana lugha, na mwingine ana fasi-ri.^b Mambo yote na yatendeke kwa ajili ya kujenga. **27** Mtu akisema kwa lugha, na wawe wawili au wasizidi watatu, na wafanye hivyo kwa zamu, na lazima mtu fulani afasiri.*^c

28 Lakini ikiwa hakuna mkalimani,* anapaswa kukaa kimya kutanikoni na kuzungumza moyoni mwake na kwa Mungu. **29** Manabii^d wawili au watatu na wazungumze, na wale wengine watambue maana. **30** Lakini ikiwa mwingine anapokea ufunuo akiwa ameketi hapo, msemaji wa kwanza anapaswa kukaa kimya. **31** Kwa maana nyote mnaweza kutoa unabii kila mtu kwa wakati wake, ili wote wajifunze na wote watiwe moyo.^e **32** Na zawadi za roho ya manabii zinapaswa kuelekezwa na manabii. **33** Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko bali ni wa amani.^f

Kama ilivyo katika makutaniko yote ya watakatifu, **34** wanawake na wakae kimya katika makutaniko, kwa maana hawaruhusiwi kuzungumza.^g Badala yake, na wajitii-she,^h kama vile Sheria inavyosema pia. **35** Ikiwa wanataka kujifunza jambo fulani, acheni wawaulize waume zao

14:27 *Au "atafsiri." 14:28 *Au "mtaf-siri."

SURA YA 14

a Isa 45:14
Zek 8:23

b 1Ko 12:8, 10

c 1Ko 14:5

d Mdo 13:1

e Ebr 10:24, 25

f 1Ko 14:40
Kol 2:5

g 1Ti 2:11, 12

h 1Ko 11:3
Efe 5:22
Kol 3:18
Tit 2:5
1Pe 3:1

Safu ya 2

a 1Th 5:20

b 1Ko 14:27

c 1Ko 14:33
Kol 2:5

SURA YA 15

d Mdo 18:1, 11

e Zb 22:15
Isa 53:8, 12
Da 9:26
1Pe 2:24

f Isa 53:9
Mt 27:59, 60

g Mt 28:7

h Yon 1:17
Lu 24:46

i Zb 16:10

j Mt 10:2
Lu 24:33, 34

k Yoh 20:26

l Mt 28:16, 17

nyumbani, kwa maana ni aibu kwa mwanamke kuzungumza kutanikoni.

36 Je, neno la Mungu lilitoka kwenu, au liliwafikia ninyi peke yenu?

37 Ikiwa yeyote anafikiri yeye ni nabii au amepewa zawadi ya roho, anapaswa kutambua kwamba mambo ninayowaandikia ni amri ya Bwana. **38** Lakini yeyote akiyapuuza, yeye pia atapuuzwa.*

39 Basi ndugu zangu, endeeleni kujitahidi kutoa unabii,^a na bado msikataze ku-sema kwa lugha.^b **40** Lakini mambo yote na yatendeke kwa adabu na kwa mpango.*^c

15 Basi akina ndugu, ninawakumbusha kuhusu habari njema niliyowatangazia,^d nanyi mkaipokea pia, na mmechukua msimamo kwa ajili yake. **2** Kupitia hiyo ninyi pia mnaokolewa ikiwa mtashika sana habari njema niliyowatangazia, isipokuwa iwe mlikuwa waamini bila kusudi.

3 Kwa maana kati ya mambo ya kwanza niliyowapa ni yale niliyopokea pia, kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kulingana na Maandiko;^e **4** na kwamba alizikwa,^f ndiyo, kwamba alifufuliwa^g siku ya tatu^h kulingana na Maandiko;ⁱ **5** na kwamba alimtokea Kefa,^{*j} kisha wale 12.^k **6** Baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya 500 kwa wakati mmoja,^l na wengi kati yao bado tuko nao, ingawa wengine wamelala usingizi katika kifo. **7** Baadaye ali-

14:38 *Au labda, "Ikiwa yeyote hajui, ataendelea kutojua." 14:40 *Au "kwa utaratibu." 15:5 *Pia anaitwa Petro.

mtokea Yakobo,^a kisha mitume wote.^b **8** Lakini mwisho kabisa alinitokea mimi pia^c kana kwamba kwa yule aliyezaliwa kabla ya wakati wake.

9 Kwa maana mimi ni mdogo zaidi kati ya mitume, nami sistahili kuitwa mtume, kwa sababu nililitesa kutaniko la Mungu.^d **10** Lakini kwa fadhili zisizostahiliwa za Mungu mimi niko kama nilivyo. Na fadhili zake zisizostahiliwa kwangu hazikuwa za bure, bali nilifanya kazi zaidi yao wote; lakini si mimi bali ni fadhili zisizostahiliwa za Mungu zilizo pamoja nami. **11** Iwe ni mimi au ni wao, hivi ndivyo tunavyohubiri, na hivyo ndivyo mlivyoamini.

12 Basi ikiwa inahubiriwa kwamba Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu,^e kwa nini wengine kati yenu wanasema hakuna ufufuo wa wafu? **13** Kwa kweli, ikiwa hakuna ufufuo wa wafu, basi Kristo hakufufuliwa. **14** Lakini ikiwa Kristo hakufufuliwa, hakika kuhubiri kwetu ni bure, na imani yenu pia ni bure. **15** Isitoshe, tunaonekana pia kuwa mashahidi wa uwongo wa Mungu,^f kwa sababu tumetoa ushahidi dhidi ya Mungu kwa kusema kwamba alimfufua Kristo,^g ambaye hakumfufua ikiwa kwa kweli wafu hawatafufuliwa. **16** Kwa maana ikiwa wafu hawatafufuliwa, basi Kristo hakufufuliwa. **17** Isitoshe, ikiwa Kristo hakufufuliwa, imani yenu ni bure; nanyi mnabaki katika dhambi zenu.^h **18** Basi pia, wale ambao wamelala usingizi katika kifo wakiwa katika muungano na Kristo wamea-

SURA YA 15

a Mdo 12:17

b Mdo 1:3, 6

c Mdo 9:3-5

d Mdo 8:3
Gal 1:13e Mdo 4:2
Mdo 17:31

f Mdo 3:15

g Mdo 2:24
Mdo 4:10
Mdo 13:30, 31h Ro 4:25
Ebr 7:25

Safu ya 2

a Mdo 7:59
1Ko 15:14
1Pe 1:3b Mdo 26:23
Kol 1:18

c Mwa 3:17, 19

d Yoh 11:25

e Ro 5:12

f Ro 5:17
Ro 6:23

g Ufu 1:5

h Mt 24:3
1Th 4:16

i Da 2:44

j Zb 110:1, 2

k Ufu 20:14

l Zb 8:6
Efe 1:22

m Ebr 2:8

n 1Pe 3:22

o Yoh 14:28

p 1Ko 3:23

q Ro 6:4

ngamia,^a **19** Ikiwa ni katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi ndio wa kusikitikiwa kuliko mtu yeyote.

20 Lakini sasa Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu, akiwa matunda ya kwanza ya wale ambao wamelala usingizi katika kifo.^b **21** Kwa kuwa kifo kilikuja kupitia mwanadamu,^c ufufuo wa wafu pia unakuja kupitia mwanadamu.^d

22 Kwa maana kama vile katika Adamu wote wanakufa,^e vivyo hivyo pia katika Kristo wote watafanywa kuwa hai.^f **23** Lakini kila mmoja kwa mpangilio wake unaofaa: Kristo aliye matunda ya kwanza,^g baadaye wale walio wa Kristo wakati wa kuwapo kwake.^h **24** Kisha, mwisho, atakapoukabidhi Ufalme kwa Mungu wake aliye Baba yake, atakapokuwa ameangamiza serikali yote na mamlaka yote na nguvu zote.ⁱ **25** Kwa maana lazima atawale akiwa mfalme mpaka Mungu atakapoweke maadui wote chini ya miguu yake.^j **26** Na adui wa mwisho atakayeangamizwa ni kifo.^k **27** Kwa maana Mungu "alivitiisha vitu vyote chini ya miguu yake."^l Lakini anaposema 'vitu vyote vimetiishwa,'^m ni wazi kwamba hilo halimhusu Yule aliyevitiisha vitu vyote chini yake.ⁿ **28** Lakini vitu vyote vitakapotiishwa kwake, ndipo Mwana mwenyewe atakapojitiisha pia kwa Yule aliyevitiisha vitu vyote kwake,^o ili Mungu awe vitu vyote kwa kila mtu.^p

29 Kama sivyo, watafanya nini wale wanaobatizwa kwa kusudi la kuwa wafu?^q Ikiwa wafu hawatafufuliwa kamwe,

kwa nini basi wanabatizwa kwa kusudi la kuwa hivyo? **30** Kwa nini sisi pia tumo haritari kila saa?^{*a} **31** Ninakabili kifo kila siku. Hili ni hakika kama ilivyo furaha yanayo kwenu, akina ndugu, niliyo nayo katika Kristo Yesu Bwana wetu. **32** Ikiwa kama watu wengine,^{*} nimepigana na wanyama wa mwituni huko Efeso,^b hilo lina faida gani kwangu? Ikiwa wafu hawatafufuliwa, “acheni tuele na tunywe, kwa maana kesho tutakufa.”^c **33** Msipotoshwe. Kushirikiana na watu wabaya huharibu tabia nzuri.^{*d} **34** Amkeni kwa njia ya uadilifu na msiwe na mazoea ya kufanya dhambi, kwa maana wengine hawamjui Mungu. Ninasema ili kuwafanya mwone aibu.

35 Hata hivyo, mtu fulani atauliza: “Wafu watafufuliwaje? Ndiyo, watakuja wakiwa na mwili wa aina gani?”^e **36** Wewe mtu usiye na akili! Kile unachopanda hakiwi hai isipokuwa kwanza kife. **37** Na kuhusu kile unachopanda, unapanda, si mwili utakaochipuka, bali ni mbe-gu tu, iwe ya ngano au mbe-gu ya aina nyingine; **38** lakini Mungu huipa mwili kama anavyopenda na huipa kila mbe-gu mwili wake. **39** Nyama zote si za aina moja, bali kuna ya wanadamu, kuna nyama ya mifugo, kuna nyama ya ndege, na nyingine ya samaki. **40** Na kuna miili ya mbinguni^f na miili ya duniani;^g lakini utukufu wa miili ya mbinguni

15:30 *Au “wakati wote.” **15:32** *Au labda, “kwa maoni ya kibinadamu.” **15:33** *Au “hupotosha maadili.”

SURA YA 15

a Ro 8:36
2Ko 11:23-27

b 2Ko 1:8

c Isa 22:13

d Met 13:20
1Ko 5:6

e 1Yo 3:2

f Mt 28:3
Lu 24:4

g Ebr 2:6, 7

Safu ya 2

a Mwa 1:16

b Ro 2:6, 7

c Kol 3:4

d Ufu 20:4

e Mwa 2:7

f Yoh 5:26
1Ti 3:16

g Mwa 2:7

h Yoh 3:13

i Flp 3:20, 21

j Mwa 5:3

k Ro 8:29

ni wa namna moja, na ule wa miili ya duniani ni wa namna nyingine. **41** Utukufu wa jua ni wa namna moja, na utukufu wa mwezi ni mwingine,^a na utukufu wa nyota ni mwingine; kwa kweli, nyota moja hutofautiana na nyota nyingine kwa utukufu.

42 Ndivyo ilivyo kuhusu ufufuo wa wafu. Hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutoweza kuharibika.^b **43** Hupandwa katika aibu; hufufuliwa katika utukufu.^c Hupandwa katika udhai-fu; hufufuliwa katika nguvu.^d **44** Hupandwa ukiwa mwili wa nyama; hufufuliwa ukiwa mwili wa roho. Ikiwa kuna mwili wa nyama, basi kuna mwili wa roho pia. **45** Basi imeandikwa hivi: “Mwanadamu wa kwanza Adamu akawa mtu aliye hai.”^{*e} Adamu wa mwisho akawa roho inayowapa watu uhai.^f **46** Hata hivyo, ule wa roho si wa kwanza. Ule wa nyama ndio wa kwanza, na baadaye ule wa roho. **47** Mtu wa kwanza ni wa kutoka duniani na ameu-mbwa kwa mavumbi;^g mtu wa pili ni wa kutoka mbinguni.^h **48** Kama yule aliyeumbwa kwa mavumbi, ndivyo wali-vyo pia wale walioumbwa kwa mavumbi; na kama alivyo yule wa mbinguni, ndivyo walivyo pia wale wa mbinguni.ⁱ **49** Na kama vile ambavyo tumechukua mfano wa yule aliyeumbwa kwa mavumbi,^j vivyo hivyo pia tutauchukua mfano wa yule wa mbinguni.^k

50 Lakini ninawaambia hivi, akina ndugu, kwamba nyama na damu haviwezi kuirithi

15:45 *Au “nafsi iliyo hai.”

Ufalme wa Mungu, wala uhari-bifu haurithi kutoweza kuha-ribika. **51** Tazama! Ninawaa-ambia siri takatifu: Hatutalala usingizi katika kifo sisi sote, bali sote tutabadilishwa,^a **52** kwa muda mfupi, kufumba na kufumbua* jicho, wa-kati wa tarumbeta ya mwisho. Kwa maana tarumbeta italia,^b na wafu watafufuliwa wakiwa wasioweza kuharibika, nasi tutabadilishwa. **53** Kwa maana huu ulio wa kuharibika la-zima uvae kutoweza kuhari-bika,^c na huu unaoweza kufa lazima uvae kutoweza kufa.^d **54** Lakini huu unaoweza ku-haribika utakapovaa kutoweza kuharibika na huu unaoweza kufa utakapovaa kutoweza kufa, ndipo neno hili lililoa-ndikwa litakapotimia: "Kifo ki-memezwa milele."^e **55** "Kifo, uko wapi ushindi wako? Kifo, uko wapi mchomo wako?"^f **56** Mchomo unaotokeza kifo ni dhambi,^g nazo nguvu za dhambi ni Sheria.*^h **57** Laki-ni tunamshukuru Mungu, kwa maana yeye hutupatia ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo!ⁱ

58 Kwa hiyo, ndugu zangu wapendwa, iweni imara,^j tha-bit, sikuzote mkiwa na mengi ya kufanya^k katika kazi ya Bwana, mkijua kwamba kazi yenu si ya bure^l kuhusiana na Bwana.

16 Basi kuhusu mchango kwa ajili ya watakatifu,^m fuateni mwongozo nili-toa kwa makutaniko ya Gala-tia. **2** Siku ya kwanza ya kila juma, kila mmoja wenu anapa-

15:52 *Au "kupepesa." 15:56 *Au "nayo Sheria huipa dhambi nguvu zake."

SURA YA 15

a 1Th 4:17

b 1Th 4:16

c Ro 2:6,7

d 2Ko 5:4

e Isa 25:8
Ufu 20:6

f Ho 13:14

g Ro 6:23

h Ro 3:20
Ro 7:12,13i Yoh 3:16
Mdo 4:12j Kol 1:23
Ebr 3:14
2Pe 3:17

k Ro 12:11

l 2Nya 15:7
1Ko 3:8
Ufu 14:13

SURA YA 16

m Mdo 24:17
Ro 15:26
2Ko 8:3,4

Safu ya 2

a 2Ko 8:19

b Mdo 19:21
2Ko 1:15,16

c Mdo 20:2

d Mdo 19:1

e Mdo 19:10,11

f Mdo 16:1,2

g Flp 2:19,20

h Mdo 18:24,25

i 1Th 5:6

j 1Ko 15:58
Flp 1:27

swa kuweka kando kitu fula-ni kulingana na uwezo wake, ili michango isikusanywe nitakapofika. **3** Lakini nita-kapofika huko, nitawatuma watu mtakaopendekeza kati-ka barua zenu,^e wapeleke za-wadi yenu ya fadhili Yerusale-mu. **4** Hata hivyo, ikiwa ita-faa mimi niende huko pia, wa-taenda pamoja nami.

5 Lakini nitakuja kwenu baada ya kupitia Makedonia, kwa maana nitapitia huko Ma-kedonia;^b **6** na labda nitakaa kwa muda au hata nitakaa na-nyi kipindi chote cha maji-ra ya baridi, ili mnisindiki-ze umbali fulani kule nitaka-poenda. **7** Kwa maana sitaki kuwaona ninyi sasa ninapopi-ta, kwa kuwa natumaini kukaa pamoja nanyi muda fulani,^c Yehova* akiruhusu. **8** Lakini nitakaa Efeso^d mpaka Shere-he ya Pentekoste, **9** kwa sa-babu nimefunguliwa mlango mkubwa unaoongoza kwenye utendaji,^e lakini kuna wapi-nzani wengi.

10 Sasa Timotheo^f akifika, hakikisheni kwamba hao-gopi chochote akiwa kati yenu, kwa maana anafanya kazi ya Yehova,^g kama mimi. **11** Kwa hiyo, mtu yeyote asi-mdharau. Msindikizeni kwa amani ili aje kwangu, kwa maana ninamsubiri nikiwa pa-moja na akina ndugu.

12 Basi kumhusu Apolo^h ndugu yetu, nilimhimiza sana aje kwenu pamoja na aki-na ndugu. Hakukusudia kuja sasa, lakini atakuja atakapo-pata nafasi.

13 Kaeni macho,ⁱ simameni imara katika imani,^j endeleeni

16:7,10 *Angalia Nyongeza A5.

kuwa kama wanaume,^{*a} iweni na nguvu.^b **14** Mambo yote mnayofanya yafanyeni kwa upendo.^c

15 Sasa ninawahimiza, aki-na ndugu: Mnajua kwamba nyumba ya Stefana ndiyo matunda ya kwanza ya Akaya na kwamba walijitoa kuwahudumia watakatifu. **16** Endeeleni kujitiisha kwa watu wa aina hiyo na kwa wale wote wanaoshirikiana na kufanya kazi kwa bidii.^d **17** Lakini ninashangilia kuwapo kwa Stefana^e na Fortunato na Akaiko, kwa sababu wamejajiza kutokuwapo kwenu hapa. **18** Kwa maana wameiburudisha roho yangu na yenu. Kwa

16:13 *Au “kuwa jasiri.”

SURA YA 16

a Mdo 4:29

b Efe 6:10
Kol 1:11

c 1Ko 13:4
1Pe 4:8

d Flp 2:29, 30
1Th 5:12
1Ti 5:17

e 1Ko 1:16

Safu ya 2

a Ro 16:3, 5
Flm 2

hiyo, watambueni watu wa namna hiyo.

19 Makutaniko ya Asia yanawatumia salamu zao. Akila na Priska pamoja na kutaniko lililo katika nyumba yao^a wanawasalimu kwa moyo mku-njufu katika Bwana. **20** Ndu-gu wote wanawasalimu. Sali-mianeni kwa busu takatifu.

21 Hii ni salamu yangu, Paulo, kwa mkono wangu mwenyewe.

22 Ikiwa yeyote hampendi Bwana, mtu huyo na alaaniwe. Njoo, Ee Bwana wetu! **23** Na muwe na fadhili zisizostahili-wa za Bwana Yesu. **24** Upe-ndo wangu na uwe pamoja na-ny nyote katika muungano na Kristo Yesu.

BARUA YA PILI KWA

WAKORINTHO

YALIYOMO

- | | |
|--|---|
| <p>1 Salamu (1, 2)
Faraja kutoka kwa Mungu katika dhiki zote (3-11)
Mabadiliko katika mipango ya safari za Paulo (12-24)</p> <p>2 Paulo akusudia kuleta shangwe (1-4)
Mtenda dhambi asamehewa na kurudishwa (5-11)
Paulo huko Troa na Makedonia (12, 13)
Huduma, maandamano ya ushindi (14-17)
Si wachuuzi wa neno la Mungu (17)</p> <p>3 Barua za mapendekezo (1-3)
Wahudumu wa agano jipya (4-6)
Utukufu ulio bora wa agano jipya (7-18)</p> <p>4 Nuru ya habari njema (1-6)
Akili za wasioamini zimepofushwa (4)
Hazina katika vyombo vya udongo (7-18)</p> | <p>5 Kuvaa makao ya kimbingu (1-10)
Huduma ya upatanisho (11-21)
Kiumbe kipya (17)
Mabalizi wa Kristo (20)</p> <p>6 Fadhili za Mungu hazipaswi kutumiwa vibaya (1, 2)
Huduma ya Paulo yafafanuliwa (3-13)
Msifungwe nira isivyo sawa (14-18)</p> <p>7 Tujisafishe unajisi (1)
Shangwe ya Paulo kuhusu Wakorintho (2-4)
Tito aleta habari nzuri (5-7)
Huzuni ya kimungu na toba (8-16)</p> <p>8 Mchango kwa ajili ya Wakristo wa Yudea (1-15)
Tito kutumwa Korintho (16-24)</p> <p>9 Wachochewa kutoa (1-15)</p> |
|--|---|

Mungu humpenda mtoaji
mchangamfu (7)

- 10 Paulo aitetea huduma yake (1-18)
Silaha zetu si za kimwili (4, 5)
- 11 Paulo na mitume walio bora sana (1-15)
Hali ngumu alizokabili Paulo akiwa
mtume (16-33)
- 12 Maono ya Paulo (1-7a)
"Mwiba katika mwili" wa Paulo (7b-10)

Hajapungukiwa kuliko mitume walio
bora sana (11-13)
Paulo awahangaikia Wakorintho (14-21)

- 13 Maonyo ya mwisho na himizo (1-14)
"Endeleeni kujijaribu kama mko
katika imani" (5)
Mrekebishwe upya; mfikiri kwa
upatano (11)

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kupitia mapenzi ya Mungu, na Timotheo^a ndugu yetu, kwa kutaniko la Mungu lililo huko Korintho, pamoja na watakatifu wote walio katika Akaya yote:^b

2 Na muwe na fadhili zizozostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

3 Asifiwe Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo,^c Baba wa rehema nyororo^d na Mungu wa faraja yote,^e **4** ambaye hutufariji* katika majaribu^f yetu yote, ili tuweze kuwafariji wengine^g walio katika majaribu^h ya namna yoyote, kwa faraja ambayo tunapokea kutoka kwa Mungu.^h **5** Kwa maana kama vile mateso kwa ajili ya Kristo yalivyo mengi ndani yetu,ⁱ ndivyo pia faraja tunayopokea kupitia Kristo ilivyo nyingi. **6** Basi tukikabili majaribu,^j ni kwa ajili ya faraja na wokovu wenu; na tukifarijiwa, ni kwa ajili ya faraja yenu inayotenda ili kuwasaidia mvumilie mateso yaleya-le ambayo sisi pia tunateseka.

1:4 *Au "hututia moyo." 1:4, 6 ^aAu "dhiki."

SURA YA 1

a Mdo 16:1, 2
Flp 2:19, 20

b 1Th 1:8

c Yoh 20:17

d Kut 34:6
Zb 86:5
Mik 7:18

e Isa 51:3
Ro 15:5

f Zb 23:4
2Ko 7:6

g Efe 6:21, 22
1Th 4:18

h Ro 15:4
2Th 2:16, 17

i 1Ko 4:11-13
Kol 1:24

Safu ya 2

a Ro 8:18
2Ti 2:11, 12

b Mdo 20:18, 19

c 1Ko 15:32

d 2Ko 12:10

e Zb 34:7, 19
2Ti 4:18
2Pe 2:9

f Flp 1:19
Flm 22

g Mdo 12:5
Ro 15:30-32

7 Na tumaini letu kwa ajili yenu haliyumbi-yumbi, kwa kuwa tunajua kwamba kama vile mnavyoshiriki katika mateso, ndivyo pia mtakavyoshiriki katika faraja.^a

8 Kwa maana hatutaki mko-se kujua, akina ndugu, kuhusu dhiki tuliyopata katika mkoa wa Asia.^b Tulikuwa na mkao wa Asia. ^b Tulikuwa na mkubwa sana unaozidi nguvu zetu wenyewe, hivi kwamba hatukuwa na uhakika hata kuhusu uhai wetu.^c

9 Kwa kweli, tulihisi kwamba tumepokea hukumu ya kifo. Ilikuwa hivyo ili tusijitegemee sisi wenyewe, bali tumtegemee Mungu^d ambaye huwafufua wafu. **10** Alituokoa kutoka katika hatari kubwa ya kifo na atatuokoa, nasi tume-weka tumaini letu kwake kwamba ataendelea kutuokoa.^e **11** Ninyi pia mnaweza kutusaidia kwa kutoa dua kwa ajili yetu,^f ili wengi wote shukrani kwa ajili yetu kwa kibali tunachopokea kwa sababu ya majibu ya sala za wengi.*^g

12 Kwa maana hili ndilo jambo tunalojisifia, dhambi yetu inatoa ushahidi kwamba tumejiendesha katika

1:11 *Au "kwa sababu ya nyuso nyingi zinazosali."

ulimwengu, na hasa kuwaelekea ninyi, kwa utakati fu na unyoofu unaotoka kwa Mungu, si kwa hekima ya kimwili,^a bali kwa fadhili zizizostahiliwa za Mungu. **13** Kwa maana kwa kweli hatuwaandikii jambo lolote isipokuwa yale mnayoweza kusoma* na kuyaelewa, nami natumaini mtaendelea kuyaelewa mambo haya kikamili,[#] **14** kama vile ambavyo pia mmelewa kwa kadiri fulani, kwamba sisi ni sababu yenu ya kujisifu, kama vile mtakavyokuwa kwetu pia katika siku ya Bwana wetu Yesu.

15 Basi nikiwa na uhakika huu, nilikusudia kuja kwenu kwanza, ili muwe na pindi ya pili ya kuwa na shangwe;* **16** kwa maana nilikusudia kuwatembelea nikiwa safarini kwenda Makedonia, nirudi kwenu baada ya kutoka Makedonia, kisha mnisindikize kwenda Yudea.^b **17** Basi, nilipokusudia hivyo, je, nilipuuza jambo hilo? Au je, mimi ninakusudia mambo kwa njia ya kimwili hivi kwamba ninasema "Ndiyo, ndiyo" na kisha "Siyo, siyo"? **18** Lakini Mungu anaweza kutegemewa ili kwamba yale tunayowambia yasiwe "ndiyo" na wakati uleule "siyo." **19** Kwa maana Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, aliyehubiriwa miongoni mwenu kupitia sisi, yaani, kupitia mimi na Silvano* na Timotheo,^c hakuwa "ndiyo" na wakati uleule "siyo," bali kuhusiana naye "ndiyo" ime-

1:13 *Au labda, "yale ambayo tayari mnayajua vizuri." [#]Tnn., "mpaka mwisho." 1:15 *Au labda, "ili mnufaike mara mbili." 1:19 *Pia anaitwa Sila.

SURA YA 1

a 1Ko 2:4, 5

b 1Ko 16:5, 6

c Mdo 18:5

Safu ya 2

a Ro 15:8

b Ufu 3:14

c 1Yo 2:20, 27

d Efe 4:30

e Ro 8:23
2Ko 5:5
Efe 1:13, 14f Ebr 13:17
1Pe 5:2, 3

SURA YA 2

g 2Ko 7:8, 9

kuwa "ndiyo." **20** Kwa maana hata ahadi za Mungu ziwe nyingi kadiri gani, zimekuwa "ndiyo" kupitia yeye.^a Kwa hiyo, kupitia yeye pia "Amina" husemwa kwa Mungu,^b nayo humletea utukufu kupitia sisi. **21** Lakini yule anayetoa uha-kikisho kwamba ninyi na sisi ni wa Kristo na yule ambaye ametutia mafuta ni Mungu.^c **22** Yeye pia ametia muhuri wake juu yetu^d naye ametupatia rehani ya kile kitakachokuja,* yaani, roho,^e katika mioyo yetu.

23 Sasa ninamwita Mungu awe shahidi dhidi yangu,* kwamba sijaja Korintho kwa sababu ya kuwahurumia ninyi. **24** Si kwamba sisi ni mabwana wa imani yenu,^f bali sisi ni wafanyakazi wenzenu kwa ajili ya shangwe yenu, kwa maana mnasimama kwa imani yenu.

2 Kwa maana nimeamua kwamba sitakuja kwenu tena kwa huzuni. **2** Kwa maana nikiwahuzunisha ninyi, ni nani atakayekuwapo ili kunichangamsha isipokuwa yule ambaye nilimhuzunisha? **3** Niliandika mambo hayo, ili, nitakapokuja, nisihuzunishwe na wale ambao ninapaswa ku-shangilia juu yao, kwa sababu nina uhakika kwamba kile kinachonipa shangwe kinawapa ninyi nyote shangwe hiyo-hiyo. **4** Kwa maana kutokana na dhiki nyingi na maumivu ya moyo niliwaandikia kwa machozi mengi, si ili niwahunzishe,^g bali niwajulishe kina cha upendo wangu kwenu.

1:22 *Au "malipo ya awali; uthibitisho (dhamana) wa kile kitakachokuja." 1:23 *Au "dhidi ya nafsi yangu."

5 Basi ikiwa yeyote amesababisha huzuni,^a hajanihuzunisha mimi, bali amewahuzunisha ninyi nyote kwa kadiri fulani—nisiwe mkali mno kwa yale ninayosema. **6** Karipio hili linalotolewa na wengi linamtosha mtu huyo; **7** bada-la yake, sasa mnapaswa kumsamehe kwa fadhili na kumfariji,^b ili asilemewe* na huzuni inayopita kiasi.^c **8** Kwa hiyo ninawahimiza ninyi kumthibitishia upendo wenu.^d **9** Ndiyo sababu niliwaandikia pia: ili kujua kama mngeonyesha uthibitisho wa utii wenu katika mambo yote. **10** Mki-samehe mtu yeyote jambo lolote, mimi pia ninamsamehe. Kwa kweli, lolote ambalo nimesamehe (ikiwa nimesamehe jambo lolote) ni kwa ajili yenu machoni pa Kristo, **11** ili Shetani asitushinde akili,^e kwa maana hatukosi kuzijua mbinu^f zake.^f

12 Basi nilipofika Troa^g kutangaza habari njema kuhusu Kristo nami nikafunguliwa mlango katika Bwana, **13** roho yangu haikupata kitulizo kwa sababu sikumkuta Tito^h ndugu yangu. Basi, nika-waaga kisha nikaondoka kwenda Makedonia.ⁱ

14 Lakini shukrani kwa Mungu, ambaye sikuzote hutuongoza katika maandamano ya ushindi kwa kushirikiana na Kristo, na kupitia sisi huieneza* harufu nzuri ya ujuzi kumhusu kila mahali! **15** Kwa maana kwa Mungu sisi ni harufu tamu ya Kristo kati ya wale wanaokole-

2:7 *Au "asimezwe." 2:11 *Au "asitudanganye." #Au "nia; njama." 2:14 *Au "huitambulisha."

SURA YA 2

a 1Ko 5:1

b Lu 15:23, 24

c Ebr 12:12

d Ro 12:10

e Lu 22:31
ZTi 2:26f Efe 6:11, 12
1Pe 5:8

g Mdo 16:8

h Gal 2:3
Tit 1:4

i 2Ko 7:5

Safu ya 2

a Yoh 15:19
2Ko 4:3
1Pe 2:7, 8

b 2Ko 4:2

SURA YA 3

c 1Ko 9:2

d 1Ko 3:5

e Kut 31:18
Kut 34:1f Met 3:3
Met 7:3g Kut 4:12, 15
Flp 2:13

h Ebr 8:6

i Ro 13:9

j Gal 3:10

k Yoh 6:63

wa na kati ya wale wanaoangamia; **16** kwa hawa wa mwisho ni harufu ya kifo inayoleta kifo,^a kwa wale wa kwanza ni harufu ya uzima inayoleta uzima. Na ni nani anayestahili kabisa mambo haya? **17** Ni sisi, kwa maana sisi si wachuuzi wa* neno la Mungu^b kama watu wengi walivyo, bali tunasema kwa unyofu wote, tukiwa tumetumwa na Mungu, ndiyo, machoni pa Mungu na kwa kushirikiana na Kristo.

3 Je, tunaanza tena kujipendekeza wenyewe? Au kama watu fulani, je, tunahitaji barua za pendekezo kuja au kutoka kwenu? **2** Ninyi wenyewe ndio barua yetu,^c iliyoandikwa juu ya mioyo yetu na kujulikana na kusomwa na wanadamu wote. **3** Kwa maana ni wazi kwamba ninyi ni barua ya Kristo ambayo tuliandika tukiwa wahudumu,^d iliyoandikwa si kwa wino bali kwa roho ya Mungu aliye hai, si juu ya mabamba ya mawe,^e bali juu ya mabamba ya nyama, juu ya mioyo.^f

4 Tuna uhakika wa namna hii kwa Mungu kupitia Kristo. **5** Si kwamba sisi wenyewe tunastahili vya kutosha kufikiri kuwa jambo lolote linotoka kwetu, bali kustahili kwetu vya kutosha hutoka kwa Mungu,^g **6** ambaye kwa kweli ametustahilisha vya kutosha kuwa wahudumu wa agano jipya,^h si wa sheria zilizoandikwa,ⁱ bali wa roho; kwa maana sheria zilizoandikwa huleta hukumu ya kifo,^j bali roho hufanya kuwa hai.^k

2:17 *Au "hatufanyi biashara; hatupati faida kutokana na."

7 Basi ikiwa sheria zinazotoa kifo ambazo zilichongwa kwa herufi kwenye mawe^a zilikuja kwa utukufu kama huo hivi kwamba wana wa Israeli hawakuweza kuutazama uso wa Musa kwa sababu ya utukufu wa uso wake,^b utukufu ambao ungekuja kuondolewa, 8 kwa nini kutolewa kwa roho^c kusiwe kwenye utukufu zaidi?^d 9 Kwa maana ikiwa sheria zilizotoa hukumu ya hatia^e zilikuwa zenye utukufu,^f kutolewa kwa uadilifu kungekuwa na utukufu mwingi kadiri gani!^g 10 Kwa kweli, hata kile ambacho wakati fulani kilifanywa kiwe na utukufu kimevuliwa utukufu, kwa sababu ya utukufu unaokizidi.^h 11 Kwa maana ikiwa kile ambacho kingeondolewa kiliingizwa kwa utukufu,ⁱ basi utukufu wa kinachobaki ungekuwa mwingi kadiri gani!

12 Kwa kuwa tuna tumaini hilo,^k tunazungumza kwa uhuru mwingi, 13 nasi hatufanyi kama Musa alivyofanya alipofunika uso wake kwa kitambaa^l ili wana wa Israeli wasitazame mwisho wa kile ambacho kingeondolewa. 14 Lakini akili zao zilitiwa uzito.^m Kwa maana mpaka leo kitambaa kilekile kinadumu bila kuondolewa agano la zamani linaposomwa,ⁿ kwa sababu kinaondolewa tu kupitia Kristo.^o 15 Kwa kweli, mpaka leo kila mara maandishi ya Musa yanaposomwa,^p kitambaa hukaa juu ya mioyo yao.^q 16 Lakini mtu anapomgeukia Yehova,^{*} kitambaa huondolewa.^r 17 Basi Yehova^{*} ni Roho,^s na mahali palipo

3:16-18 * Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 3

- a Kut 31:18
Kut 32:16
b Kut 34:29, 30
c Mdo 2:1, 4
d 1Pe 4:14
e Kum 27:26
f Kut 34:35
g Ro 3:21, 22
h Kol 2:16, 17
i Kut 19:16
Kut 24:17
j Ebr 12:22-24
k 1Pe 1:3, 4
l Kut 34:33-35
m Ro 11:7
n Yoh 12:40
o Ro 7:6
Efe 2:15
p Mdo 15:21
q Ro 11:8
r Kut 34:34
s Yoh 4:24

Safu ya 2

- a Isa 61:1
Ro 6:14
Ro 8:15
Gal 5:1, 13
b 2Ko 4:6
Efe 4:23, 24
Efe 5:1

SURA YA 4

- c 2Ko 2:17
Gal 1:9
d 2Ko 6:3, 4
e Yoh 14:30
Efe 2:2
1Yo 5:19
f 2Ko 11:14
g Kol 1:15
Ebr 1:3
h Isa 60:2
Yoh 8:12
i Mwa 1:3
j 1Pe 2:9

na roho ya Yehova,^{*} pana uheru.^a 18 Na sisi sote, tunapotoa kama vioo mrudisho wa utukufu wa Yehova^{*} tukiwa na nyuso zisizo na kitambaa, tunageuzwa kuwa katika mfano uleule kutoka kiwango kimoja cha utukufu mpaka kingine,[#] sawa na anavyofanya Yehova^{*} ambaye ni Roho.^{Ab}

4 Kwa hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii kupitia rehema tuliyoonyeshwa, hatufi moyo. 2 Hata hivyo, tumeyakataa mambo ya kichinichini ya aibu, hatutembeji kwa ujanja, au kulichanganya na kitu chochote neno la Mungu;^c bali kwa kufanya kweli iwe wazi, tunajipendekeza kwa kila dhamiri ya mwanadamu machoni pa Mungu.^d 3 Ikiwa kwa kweli habari njema tunayotangaza imefunikwa kwa kitambaa, imefunikwa kati ya wale wanaoangamia, 4 ambao kati yao mungu wa mfumo huu wa mambo^{*e} amezipofusha akili za wasioamini,^f ili nuru ya[#] habari njema yenye utukufu kuhusu Kristo, aliye mfano wa Mungu,^g isiwaangazie.^h 5 Kwa maana tunahubiri, si kuhusu sisi wenyewe, bali kuhusu Yesu Kristo kwamba ni Bwana na sisi wenyewe kwamba ni watumwa wenu kwa ajili ya Yesu. 6 Kwa maana Mungu ndiye aliyesema: “Nuru na iangaze kutoka katika giza,ⁱ naye ameangaza juu ya mioyo yetu ili kuimulika^j kwa ujuzi wenye utukufu kumhusu Mungu kupitia uso wa Kristo.

3:18 [#]Tnn., “kutoka utukufu mpaka utukufu.” [^]Au labda, “kupitia roho ya Yehova.” 4:4 ^{*} Angalia Kamusi, uku. 2012, “Mfumo wa mambo.” [#]Au “mwangaza wa.”

7 Hata hivyo, tuna hazina hii^a katika vyombo vya udongo,^{*b} ili nguvu zinazopita zile za kawaida ziwe za Mungu na si kutoka kwetu.^c **8** Tunakandamizwa katika kila njia, lakini hatubanwi kupita kiasi cha kushindwa kusonga; tunafadhaishwa, lakini si bila njia ya kutokea kabisa;^{*d} **9** tunateswa, lakini hatuachwi bila msaada;^e tunaangu-shwa chini, lakini hatuanga-mizwi.^f **10** Sikuzote katika mwili wetu tunavumilia mate-ndo yenye kuleta kifo ambayo Yesu aliteseka,^g ili uzima wa Yesu ufunuliwe pia kati-ka mwili wetu. **11** Kwa maana sikuzote sisi tunaishi tunakabili kifo uso kwa uso^h kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu ufunuliwe pia kati-ka mwili wetu unaoweza kufa. **12** Kwa hiyo kifo kinafanya kazi ndani yetu, lakini uzima ndani yenu.

13 Basi kwa sababu tuna roho ileile ya imani kama ile iliyoandikwa hivi kuihusu: "Mimi nilionyesha imani, kwa hiyo nikasema";ⁱ sisi pia tunaonyesha imani na kwa hiyo tunasema, **14** tukijua kwamba Yule aliyemfufua Yesu atatufufua sisi pia pamoja na Yesu naye atatokeza sisi pamoja nanyi.^j **15** Kwa maana mambo yote haya ni kwa ajili yenu, ili fadhili zizizostahiliwa zinazoongezeka zizidi kuwa nyingi kwa sababu wengi zaidi wanatoa shukrani kwa utukufu wa Mungu.^k

16 Kwa hiyo, hatufi moyo, lakini hata ikiwa mtu tuliye

4:7 *Au "katika mitungi ya udongo."
4:8 *Au labda, "tukiwa tumekata tamaa."

SURA YA 4

a 2Ko 4:1

b Isa 64:8
Mdo 9:15
1Ko 15:47c 2Ko 12:9,10
Flp 4:13

d 1Ko 10:13

e Ebr 13:5

f Ufu 2:10

g Flp 3:10
1Pe 4:13h Ro 8:36
1Ko 4:9
1Ko 15:31

i Zb 116:10

j 1Ko 6:14

k 2Ti 2:10

Safu ya 2

a Mt 5:12
Ro 8:18b 2Ko 5:7
Ebr 11:1

SURA YA 5

c 2Pe 1:13,14

d 1Ko 15:50
Flp 3:20,21e Ro 6:5
Ro 8:23
1Ko 15:48,49f 1Ko 15:43,44
Flp 1:21

g 1Pe 1:3,4

h Efe 2:10

i Ro 8:23
Efe 1:13,14

j Yoh 14:3

kwa nje anachakaa, hakika mtu tuliye kwa ndani anafanywa upya siku kwa siku. **17** Kwa maana ingawa dhiki* ni ya muda mfupi na ni nyepesi, inatokeza kwa ajili yetu utukufu ulio mkuu[#] na bora zaidi na zaidi, na wa milele;^a **18** huku tukikaza macho yetu, si juu ya vitu vina-vyoonekana, bali juu ya vitu visivyoonekana.^b Kwa maana vitu vinavyoonekana ni vya muda, lakini vitu visivyoonekana ni vya milele.

5 Kwa maana tunajua kwamba nyumba yetu ya kidunia, hema hili, likiharibiwa,^{*c} tutapata jengo kutoka kwa Mungu, nyumba ya milele mbinguni, ambayo haijajengwa kwa mikono.^d **2** Kwa maana tunaogua kwelikweli katika nyumba hii,^{*} tukitamani sana kuvaa ile yetu[#] kutoka mbinguni,^{△e} **3** ili kwamba tutakapoivaa, hatutapatikana tukiwa uchi. **4** Kwa kweli, sisi tulio katika hema hili tunaogua, tukilemewa kwa sababu hatutaki kuuvua huu, bali tunataka kuuvaa ule mwingine,^f ili uhai ukimeze kile kinachoweza kufa.^g **5** Basi yule aliyetutayarisha kwa ajili ya jambo hili ni Mungu,^h ambaye alitupatia roho kama rehani ya kile kitakachokuja.^{*i}

6 Basi sikuzote sisi tuna uhodari mwingi na tunajua kwamba tukiwa na makao yetu katika mwili, hatupo mahali alipo Bwana,^j **7** kwa maana tunatembea kwa imani, si kwa

4:17 *Au "majaribu." #Tnn., "ulio na uzito." 5:1 *Au "likivunjwa." 5:2 *Au "makao haya." #Au "kuvaa makao yetu." △Au "makao yetu ya mbinguni." 5:5 *Au "malipo ya awali; uthibitisho (dhamana) wa kile kitakachokuja."

kuona. **8** Lakini sisi tuna uhodari mwingi na tungependelea tusiwepo katika mwili bali tuyafanye makao yetu pamoja na Bwana.^a **9** Basi iwe ni nyumbani pamoja naye au tuspokuwa pamoja naye, lengo letu ni kukubalika kwa ke. **10** Kwa maana lazima sisi sote tusimame* mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apate malipo kulingana na mambo aliyotenda akiwa katika mwili, yawe mema au mabaya.^{#b}

11 Kwa hiyo, kwa kuwa tunajua kumwogopa Bwana, tunaendelea kuwashawishi watu, lakini tunafahamika vizuri* kwa Mungu. Hata hivyo, ninatumaini kwamba tunafahamika vizuri* pia kwa dhamiri zenu. **12** Hatujipe ndekezi wenyewe tena kweni, bali tunawapa kichocho cha kujisifu kuhusiana nasi, ili muweze kujibu wale wanaojisifu kuhusu sura ya nje^c bali si kuhusu yaliyo moyoni. **13** Kwa maana ikiwa tulikuwa tumerukwa na akili,^d ilikuwa ni kwa ajili ya Mungu; ikiwa tuna akili timamu, ni kwa ajili yenu. **14** Kwa maana upendo alio nao Kristo hutuchochea, kwa sababu tumefikia uamuzi huu, kwamba mtu mmoja alikufa kwa ajili ya wote;^e hivyo basi, wote walikuwa wamekufa. **15** Naye alikufa kwa ajili ya wote ili wale wanaoishi wasiishi tena kwa ajili ya yule aliyekufa kwa ajili yao na kufufuliwa.

16 Basi tangu sasa hatumjui mtu yeyote kulingana na

5:10 *Au "tufunuliwe." #Au "maovu."
5:11 *Au "tumefunuliwa."

SURA YA 5

a Flp 1:23

b Ufu 22:12

c 2Ko 10:10

d 2Ko 11:1, 16

e Isa 53:10
Mt 20:28
1Ti 2:5, 6

f Ro 14:7, 8

Safu ya 2

a Mt 12:50

b Yoh 20:17

c Gal 6:15

d Ro 5:10
Efe 2:15, 16
Kol 1:19, 20

e Mdo 20:24

f Ro 5:6
1Yo 2:1, 2g Ro 4:25
Ro 5:18h Mt 28:19, 20
Mdo 13:38, 39

i Efe 6:19, 20

j Flp 3:20

k Ebr 4:15
Ebr 7:26

l Ro 1:16, 17

SURA YA 6

m 2Ko 5:20

n Ro 2:4

o Isa 49:8

maoni ya kimwili.^a Hata kama wakati fulani tulimjua Kristo kulingana na mwili, kwa haka hatumjui tena kwa njia hiyo.^b **17** Kwa hiyo, ikiwa yeyote yuko katika muungano na Kristo, yeye ni kiumbe kipya;^c mambo ya zamani yalipitilia mbali; tazama! mambo mapya yamekuja kuwapo. **18** Lakini mambo yote yame-toka kwa Mungu, aliyetupa-tanisha sisi kwake mwenyewe kupitia Kristo^d na kutupa-tia huduma ya upatanisho,^e **19** yaani, kwamba Mungu kupitia Kristo alikuwa akiupata-nisha ulimwengu kwake mwenyewe,^f bila kuwahesabia makosa yao,^g naye alitukabidhi ujumbe wa upatanisho.^h

20 Kwa hiyo sisi ni mabaloziⁱ walio badala ya Kristo,^j kana kwamba Mungu alikuwa akisihi kupitia sisi. Kama walio badala ya Kristo, tunao-mba: "Mpatanishwe na Mungu." **21** Yule ambaye haku-jua dhambi^k alimfanya kuwa dhambi* kwa ajili yetu, ili kupitia yeye tuwe uadilifu wa Mungu.^l

6 Huku tukifanya kazi pamoja naye,^m tunawahimi-za pia msipokee fadhili zisizo-stahiliwa za Mungu na kuko-sa kusudi lake.ⁿ **2** Kwa ma-na anasema: "Katika wakati unaokubalika nilikusikia, na katika siku ya wokovu niliku-saidia."^o Tazama! Sasa ndio wakati unaokubalika hasa. Ta-zama! Sasa ndiyo siku ya wokovu.

3 Hatutoi sababu yoyote ya kukwaza, ili kosa lolote lisipatikane katika huduma

5:21 *Au "dhabihu ya dhambi."

yetu;^a **4** bali katika kila njia tunajipendekeza kuwa wahu-dumu wa Mungu,^b kwa kuvu-milia mengi, kwa dhiki, kwa nyakati za uhitaji, kwa shi-da,^c **5** kwa kupigwa, kwa ku-fungwa gerezani,^d kwa ma-chafuko, kwa kazi ngumu, kwa kukosa usingizi usiku, kwa nyakati za kukosa chaku-la;^e **6** kwa utakaso, kwa uju-zi, kwa subira,^f kwa fadhili,^g kwa roho takatifu, kwa upen-do usio na unafiki,^h **7** kwa kusema maneno ya kweli, kwa nguvu za Mungu;ⁱ kupi-tia silaha za uadilifu^j katika mkono wa kulia* na wa ku-shoto,[#] **8** kupitia utukufu na aibu, kupitia habari mbaya na habari nzuri. Tunaonwa kuwa wadanganyifu na bado tunasema ukweli, **9** kama wasiojulikana na bado tuna-tambuliwa, kama wanaokufa* na bado, tazama! tunaishi,^k kama walioadhibiwa[#] na bado hatujakabidhiwa kwenye kifo,^l **10** kama walio na huzuni la-kini wanaoshangilia sikuzote, kama maskini lakini wanao-watajirisha wengi, kama wasio na kitu chochote na bado walio na vitu vyote.^m

11 Tumefungua kinywa chetu ili kuzungumza* nanyi, enyi Wakorintho, nasi tumefungua wazi moyo wetu. **12** Hatujajizua* kuwaonyesha upendo,ⁿ bali ninyi mmeji-zuia kutuonyesha upendo wenu mwororo. **13** Kwa hiyo, kwa kujibu—ninazungumza

6:7 *Labda kwa ajili ya kushambulia. #Labda kwa ajili ya kujilinda. 6:9 *Au "tunaonwa kama wanaostahili kifo." #Au "waliotiwa nidhamu." 6:11 *Au "Tumezungumza waziwazi." 6:12 *Au "Hatujakosa nafasi ya."

SURA YA 6

a 1Ko 9:22
b 2Ko 4:1, 2
c 2Ko 11:23
d Ufu 2:10
e 2Ko 11:25, 27
f Kol 3:13
1Th 5:14
g Efe 4:32
h Ro 12:9
i 1Ko 2:4, 5
j 2Ko 10:4
Efe 6:11
k 2Ko 4:10, 11
l Mdo 14:19
2Ko 4:8, 9
m Flp 4:13
Ufu 2:9
n 2Ko 12:15

Safu ya 2

a 1Pe 2:17
1Yo 4:20
b Kut 23:32, 33
Kum 7:3, 4
1Fa 11:4
1Ko 7:39
c Yak 4:4
d Efe 5:7, 8
e Mt 4:10
Ufu 12:7, 8
f 1Ko 10:21
g 1Ko 10:14
h 1Ko 3:16
i Kut 29:45
j Law 26:11, 12
Eze 37:27
k Isa 52:11
Yer 51:45
Ufu 18:4
l Eze 20:41
2Ko 7:1
m 2Sa 7:14
n Isa 43:6
Ho 1:10
Yoh 1:12

SURA YA 7

o 2Ko 6:16
p Ro 12:1
1Ti 1:5
1Ti 3:9
1Yo 3:3
q Ro 12:10
2Ko 6:12, 13
r Mdo 20:33, 34
2Ko 12:17

kama na watoto wangu—ninyi pia fungueni kabisa mioyo yenu.*^a

14 Msifungwe nira* isivyo sawa pamoja na wasio waami-ni.^b Kwa maana kuna ushirika gani kati ya uadilifu na uasi sheria?^c Au nuru ina ushirika gani na giza?^d **15** Isitoshe, kuna upatano gani kati ya Kri-sto na Beliali?^{*e} Au mwami-ni[#] ana ushirika gani^Δ na mtu asiye mwamini?^f **16** Na hekalu la Mungu lina makubaliano gani na sanamu?^g Kwa maa-na sisi ni hekalu la Mungu ali-ye hai;^h kama Mungu alivyo-sema: "Mimi nitakaa miongoni mwaoⁱ na kutembea miongo-ni mwao, nami nitakuwa Mun-gu wao, nao watakuwa watu wangu."^j **17** "Kwa hiyo, to-keni miongoni mwao na mji-tenge," asema Yehova,* 'na mwache kugusa kitu kicha-fu'";^k "nami nitawakaribisha ndani."^l **18** "Nami nitaku-wa baba kwenu,^m nanyi mta-kuwa wana na mabinti kwa-ngu,"ⁿ asema Yehova,* Mweza Yote."

7 Kwa hiyo, wapendwa, kwa kuwa tuna ahadi hizi,^o acheni tujisafishe kila unajisi wa mwili na roho,^p tukiukam-lisha utakatifu katika kumwo-gopa Mungu.

2 Tupatieni nafasi mioyoni mwenu.^q Hatujamkosea yeyo-te, hatujamharibu yeyote, ha-tujamdanganya yeyote ili tu-pate faida.^r **3** Sisemi jambo

6:13 *Au "ninyi pia panukeni." 6:14 *Au "Msiunganishwe." 6:15 *Kutoka-na na neno la Kiebrania linalomaanisha "Asiyefaa Kitu." Linamrejelea Shetani. #Au "mtu mwaminifu." ΔAu "mwami-ni ana fungu gani." 6:17, 18 *Angalia Nyongeza A5.

hili ili niwahukumu. Kwa maana tayari nimesema kwamba ninyi mko ndani ya mioyo yetu ili kufa pamoja na kuishi pamoja. **4** Nina uhuru mwingi wa kusema kuwaeleka ninyi. Ninajisifu sana kuhusiana nanyi. Nimejawa na faraja; ninafurika shangwe katika taabu yetu yote.^a

5 Kwa kweli, tulipofika Makedonia,^b miili yetu haikupata kitulizo, bali tuliendelea kutaabishwa katika kila njia—nje kulikuwa na mapigano na ndani woga. **6** Lakini Mungu, ambaye huwafariji wale waliovunjika moyo,^c alitufariji kwa kuwapo kwa Tito; **7** na si kwa kuwapo kwake tu bali pia kwa faraja ambayo alipokea kwa sababu yenu, kwa kuwa alirudi na kutujulisha kuhusu tamaa yenu ya kuniona, huzuni yenu nyingi, na jinsi mlivyonihangaikea sana;* hivyo nikashangilia hata zaidi.

8 Kwa maana hata kama niliwahuzunisha kwa barua yangu,^d sijuti kuhusu jambo hilo. Ingawa mwanzoni nilijuta (nilipoona kwamba barua hiyo iliwahuzunisha, ingawa ni kwa muda mfupi tu), **9** sasa ninashangilia, si kwa sababu mlihuzunishwa tu, bali kwa sababu mlihuzunishwa hivi kwamba mkatubu. Kwa maana mlihuzunishwa kwa njia ya kimungu, kwa hiyo hamkupata madhara kwa sababu yetu. **10** Kwa kuwa huzuni kwa njia ya kimungu hutokeza toba inayongoza kwenye wokovu, bila kuleta majuto;^e lakini huzu-

7:7 *Tnn., "bidii yenu kwa ajili yangu."

SURA YA 7

a Flp 2:17
Flm 7

b Mdo 20:1

c 2Ko 1:3, 4

d 2Ko 2:4

e Zb 32:5
1Yo 1:9

Safu ya 2

a Mt 3:8

b 1Ko 5:5

c 2Ko 2:9
Ebr 13:17

SURA YA 8

d Ro 15:26

ni ya ulimwengu hutokeza kifo. **11** Kwa maana, ona jinsi kuhuzunishwa kwenu kwa njia ya kimungu kulivyotokeza bidii nyingi ndani yenu, ndiyo, mljiondolea hatia, ndiyo, ghadhabu, ndiyo, woga, ndiyo, kutamani sana,* ndiyo, bidii, ndiyo, kurekebisha kosa!^a Katika kila njia mljionyesha kuwa safi[#] kuhusu jambo hili. **12** Ingawa niliwaandikia, sikufanya hivyo kwa ajili ya yule aliyefanya kosa,^b wala kwa ajili ya yule aliyekosewa, bali ili bidii yenu kwa ajili yetu ithibitishwe miongoni mwenu machoni pa Mungu. **13** Ndiyo sababu tumefarijiwa.

Lakini kwa kuongezea faraja yetu, tulishangilia hata zaidi kuhusu shangwe ya Tito, kwa sababu ninyi nyote mliiburudisha roho yake. **14** Kwa maana ikiwa nimejisifu kwake juu yenu, sijapata aibu; lakini kama vile mambo tuliyowaambia yalivyokuwa ya kweli, ndivyo pia kujisifu kwetu kwa Tito kumekuwa kweli. **15** Pia, upendo wake mwororo kwenu ni mwingi anapokumbuka utii wenu nyote,^c jinsi mlivyompokea kwa kuogopa na kutetemeka. **16** Ninashangilia kwamba katika kila njia nitakuwa na uhakika kuwahusu ninyi.*

8 Basi akina ndugu, tunawajulisha kuhusu fadhili zizozostahiliwa za Mungu ambazo makutaniko ya Makedonia^d yamepewa. **2** Wakati wa majaribu makali chini ya mateso,

7:11 *Au "kutamani sana kutubu." [#]Au "safi kiadili; bila hatia." 7:16 *Au labda, "nitakuwa na ujasiri mwingi kwa sababu yenu."

shangwe yao nyingi na umaskini mkubwa ulifanya utajiri wa ukarimu wao uwe mwingi.*

3 Kwa maana ilikuwa kulingana na uwezo wao,^a ndiyo, ninashuhudia, hata kupita uwezo wao,^b **4** nao kwa kupenda kwao wenyewe waliendelea kutuomba sana wapate pendeleo la kutoa kwa fadhili, ili washiriki katika huduma ya kutoa msaada kwa ajili ya watakatifu.^c **5** Na si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa wenyewe kwa Bwana na kwetu kupitia mapenzi ya Mungu. **6** Basi tukamtia moyo Tito^d kwamba kama vile alivyokuwa ameanzisha kazi hii kati yenu, pia akamilishe utoaji huu wenye fadhili kwa upande wenu. **7** Hata hivyo, kama vile mlivyo na utajiri katika kila jambo, katika imani na neno na ujuzi na bidii yote na katika upendo wetu kwenu, pia mzidi katika utoaji huu wenye fadhili.^e

8 Sisemi hivi ili kuwaamuru, bali kuwajulisha kuhusu bidii ya wengine na kuujaribu uhalisi wa upendo wenu. **9** Kwa maana mnazijua fadhili zisizostahiliwa za Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba ingawa alikuwa tajiri, alikuja kuwa maskini kwa ajili yenu,^f ili muwe matajiri kupitia umaskini wake.

10 Kuhusu jambo hili ninatoa maoni yangu:^g Hii ni kwa ajili ya faida yenu, kwa kuwa tayari mwaka mmoja uliopita hamkuchukua tu hatua, bali pia mlionyesha tamaa ya kufanya hivyo. **11** Hivyo basi, malizeni pia kile mlichianza kufanya, ili utaya-

SURA YA 8

a Mdo 11:29
2Ko 9:7

b Mk 12:43, 44

c Ro 15:25, 26
1Ko 16:1
2Ko 9:1, 2

d 2Ko 12:18

e 1Ti 6:18

f Mt 8:20
Flp 2:7

g 1Ko 7:25

Safu ya 2

a Kum 16:10, 17
Met 3:27, 28

b Kut 16:18

c 2Ko 12:18

d 1Ko 16:1

e Met 3:4
1Pe 2:12

ri wenu wa kutenda ukamilishwe kulingana na uwezo mlio nao. **12** Kwa maana ikiwa utayari upo kwanza, hukubalika zaidi kulingana na kile ambacho mtu anacho,^a si kulingana na kile ambacho mtu hana. **13** Kwa maana sitaki kufanya iwe rahisi kwa wengine, lakini vigumu kwenu; **14** bali kwamba kupitia usawazisho, ziada yenu kwa sasa ijazie uhitaji wao, ili ziada yao pia ijazie upungufu wenu, ili kuwe na usawazisho. **15** Kama ilivyoandikwa: "Mtu aliyekuwa na vingi hakuwa na vingi mno, na mtu aliyekuwa na vichache hakuwa na vichache mno."^b

16 Basi shukrani kwa Mungu kwa kumfanya Tito awahangaikie ninyi kwa bidii ileile kutoka moyoni,^c **17** kwa sababu kwa kweli ameitikia tulipomtia moyo, lakini akiwa mwenye bidii sana, anakuja kwenu kwa kupenda kwake mwenyewe. **18** Lakini pamoja naye tunamtuma ndugu ambaye sifa yake kuhusiana na habari njema imeenea katika makutaniko yote. **19** Si hayo tu, bali pia makutaniko yalimweka rasmi asafiri pamoja nasi tunaposhughulikia zawadi hii ya fadhili kwa ajili ya utukufu wa Bwana na kwa uthibitisho wa utayari wetu wa kusaidia. **20** Hivyo, tunaepuka kulamiwa na mtu yeyote kuhusiana na mchango huu wa ukarimu ambao tunaushughulikia.^d **21** Kwa maana 'tunaushughulikia mambo yote kwa unyoofu, si machoni pa Yehova* tu bali pia machoni pa wamadamu.'^e

8:2 *Au "ufurike."

8:21 *Angalia Nyongeza A5.

22 Zaidi ya hayo, pamoja nao tunamtuma ndugu yetu ambaye mara nyingi tumemjaribu na kuona ana bidii katika mambo mengi, lakini sasa ana bidii nyingi zaidi kwa sababu ya uhakika wake mku-bwa kwenu. **23** Ingawa hivyo, kama kuna swali lolote kumhusu Tito, yeye ni mwenzangu* na mfanyakazi mwenzi kwa ajili ya faida yenu; au kama kuna swali kuhusu ndugu zetu, wao ni mitume wa makutaniko na utukufu wa Kristo. **24** Basi thibitisheni upendo wenu kwao,^a na mwnyeshe makutaniko sababu iliyofanya tujisifu kuwahusu ninyi.

9 Basi kuhusu huduma ambayo ni kwa ajili ya watakatifu,^b kwa kweli si lazima niwaandikie ninyi, **2** kwa maana ninajua utayari wenu ambao ninajisifia kwa Wamakedonia, kwamba Akaya imekuwa tayari kwa mwaka mmoja sasa, na bidii yenu imewachochea wengi kati yao. **3** Lakini ninawatuma akina ndugu, ili kujisifu kwetu juu yenu kusiwe bure kuhusiana na jambo hilo, na kwamba muwe tayari kwelikweli, kama nilivyosema mtakuwa. **4** La sivyo, Wamakedonia wakija pamoja nami na kukuta hamko tayari, sisi—nanyi pia—tutaona aibu kwa sababu ya uhakika wetu kwenu. **5** Basi niliona ni jambo muhimu kuwatia moyo akina ndugu watangulie kuja kwenu na kuitayarisha mapema zawadi yenu ya ukarimu iliyoahidiwa, ili iwe tayari kama zawadi ya

8:23 *Tnn., "mshiriki."

SURA YA 8

a 1Pe 1:22
1Pe 2:17

SURA YA 9

b Ro 15:26
1Ko 16:1
2Ko 9:12

Safu ya 2

a Met 11:24
Met 19:17
Met 22:9
Mhu 11:1
Lu 6:38

b Kum 15:7,10

c Kut 22:29
Met 11:25
Mdo 20:35
Ebr 13:16

d Met 28:27
Mal 3:10
Flp 4:18,19

e Zb 112:9

f Ro 15:26,27
2Ko 8:14

ukarimu, bali si kama kitu cha kulazimishwa.

6 Lakini kuhusu hili, yeyote anayepanda kwa uhaba atavuna pia kwa uhaba, naye anayepanda kwa wingi atavuna pia kwa wingi.^a **7** Kila mmoja na afanye kama alivyoazimia moyoni mwake, si kwa kutopenda* wala kwa kulazimishwa,^b kwa maana Mungu humpenda mtoaji mchangamfu.^c

8 Isitoshe, Mungu anaweza kufanya fadhili zake zote zisizostahiliwa ziwe nyingi kuwaelekea, ili sikuzote muwe na vitu vya kuwatosheleza kabisa katika kila jambo, na pia muwe na vingi kwa ajili ya kila kazi njema.^d **9** (Kama ilivyoandikwa: "Amegawa kwa wingi;* amewapa maskini. Uadilifu wake unadumu milele."^e

10 Basi Yule ambaye humgawia mpandaji mbegu kwa wingi na mkate wa kula atawingawia na kuwazidishia ninyi mbegu ili mzipande naye ataongeza mavuno ya uadilifu wenu.) **11** Katika kila jambo mnatajirishwa kwa ajili ya kila namna ya ukarimu, ambao kupitia kwetu hufanya watu wamshukuru Mungu; **12** kwa kuwa huduma ya utumishi huu wa watu wote si kuandaa vizuri tu mahitaji ya watakatifu' bali pia kuwe na utajiri wa shukrani nyingi kwa Mungu. **13** Kupitia uthibitisho wa huduma hii ya kutoa msaada, wanamtukuza Mungu kwa sababu mnajitiisha kwenye habari njema kumhusu Kristo, kama mlivyotangaza hadharani, na kwa sababu ninyi ni wakarimu katika mchango wenu

9:7 *Au "bila kutaka." 9:9 *Au "kwa ukarimu."

kwao na kwa wote.^a **14** Na kupitia dua kwa ajili yenu, wanaonyesha upendo wao kweni kwa sababu ya fadhili nyingi zisizostahiliwa za Mungu juu yenu.

15 Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya zawadi yake ya bure isiyoelezeka.

10 Basi mimi mwenyewe, Paulo, ninawasihi kwa upole na fadhili za Kristo,^b ingawa mimi ni wa hali ya chini ninapokuwa kati yenu uso kwa uso,^c lakini jasiri kuwaelekea ninyi nisipokuwapo.^d **2** Ninaomba kwamba nitakapokuwapo, nisilazimike kuwa jasiri na kuchukua hatua kali ambazo ninakusudia dhidi ya wale wanaotuona kana kwamba tulitembea kwa njia ya kimwili. **3** Kwa maana ingawa tunatembea katika mwili, hatupigani vita kulingana na vile tulivyo katika mwili. **4** Kwa maana silaha za vita vyetu si za kimwili,^e bali ni zenye nguvu kupitia Mungu^f kwa ajili ya kuzipindua ngome zenye nguvu. **5** Kwa maana tunapindua mawazo na kila jambo lililo juu sana ambalo limeinuliwa kinyume cha ujuzi wa Mungu,^g nasi tunaiteka kila fikira ili kuifanya imtii Kristo; **6** nasi tuko tayari kutoa adhabu kwa ajili ya kila tendo la kutotii,^h mara tu utii wenu utakapokamilika.

7 Mnayatazama mambo kulingana na thamani yake ya nje. Mtu yeyote akijiamini kwamba yeye ni wa Kristo, acheni afikirie tena jambo hili: Kama vile yeye alivyo wa Kristo, ndivyo na sisi pia. **8** Kwa maana hata ni-

SURA YA 9

a Mt 5:16
Ebr 13:16
Yak 1:27
1Yo 3:17

SURA YA 10

b Mt 11:29, 30

c 1Ko 2:3

d 2Ko 10:10

e Mt 26:52
1Ti 1:18, 19

f 2Ko 6:4, 7

g 1Ko 1:19, 20
1Ko 3:19, 20
2Ti 2:24, 25

h 1Ti 1:20

Safu ya 2

a Ebr 13:17

b 2Ko 13:2

c 2Ko 5:12

d Met 26:12
Gal 6:3

e Mdo 9:15
Gal 2:8

f 1Ko 3:10
1Ko 4:15

kijisifu sana kuhusu mamla-ka ambayo Bwana alitupa-tia ili tuwajenge wala si ku-wabomoa ninyi,^a mimi sitaai-bishwa. **9** Kwa maana sitaki ionekana kama ninajaribu kuwatisha kwa barua za-angu. **10** Kwa maana wanase-ma: "Barua zake ni nzito na zenye nguvu, lakini akiwapo yeye mwenyewe, ni dhafu na maneno yake ni yenye kudha-raulika." **11** Mtu kama huyo ajue kwamba mambo tunayo-sema* kupitia barua tusipoku-wapo, tutayafanya pia[#] tuta-kapokuwapo.^b **12** Kwa ma-na sisi hatuthubutu kujiweka katika kikundi au kujilinga-nisha na watu fulani wanao-jipendekeza wenyewe.^c Lakini wanapojipima wenyewe kwa wenyewe na kujilinganisha wenyewe kwa wenyewe, hawa-na uelewaji.^d

13 Hata hivyo, hatutajisifu nje ya mipaka tuliyogawiwa, bali katika mpaka wa eneo ambalo Mungu alitupimia,^{*} na kuufanya ufike hadi kwe-nu.^e **14** Kwa kweli, sisi hatuvuki mpaka wetu kana kwamba hatukuwafikia ninyi, kwa maana tulikuwa wa kwanza kufika hadi kwenu tuki-wa na habari njema kuhusu Kristo.^f **15** Hapana, hatujisi-fu kuhusu kazi za mtu mwi-ngine nje ya mipaka tuliyoga-wiwa, bali tunatumaini kwa-amba imani yenu inapozidi kuongezeka, mambo tuliyofa-nya yatazidi kuongezeka kati-ka eneo letu. Ndipo tutazidi hata zaidi, **16** ili tutangaze

10:11 *Tnn., "jinsi tulivyo katika mane-no." [#]Tnn., "tutakuwa hivyo pia katika matendo." **10:13** *Au "alitugawia kwa kipimo."

habari njema katika nchi zilizo ng'ambo yenu, na hivyo tusijisifu kuhusu mambo ambayo tayari yamefanywa katika eneo la mtu mwingine. **17** "Lakini yule anayejisifu, na ajisifu katika Yehova."^a **18** Kwa maana si yule anayejipendekeza ambaye hukubaliwa,^b bali ni yule ambaye Yehova* humpendekeza.^c

11 Laiti mngenivumilia katika kukosa kidogo akili. Lakini kwa kweli, mnanimvumilia! **2** Kwa maana nina wivu juu yenu, wivu wa kimungu,* kwa kuwa mimi binafsi niliwachumbia mume mmoja ili niwatoe mkiwa bikira safi[#] kwa Kristo.^d **3** Lakini kwa njia fulani, ninaogopa kwanamba kama nyoka alivyomshawishi Hawa kwa ujanja,^e huenda akili zenu zikapotoshwa kutoka kwenye unyoofu wa moyo na usafi* nao-mfaa Kristo.^f **4** Kwa maana, kama ilivyo, mtu akija na kuhubiri Yesu mwingine tofauti na yule tuliymhubiri, au mkipokea roho nyingine tofauti na ile mliyopokea,^g au habari njema nyingine tofauti na ile mliyokubali, mnakubaliana naye. **5** Kwa maana ninana kwamba katika jambo lolote sijawa mdogo kuliko mitume wenu walio bora sana.^h **6** Lakini hata kama sina ustadi wa kusema,ⁱ hakika nina ujuzi; kwa kweli tuliwafanulia katika kila njia na katika mambo yote.

7 Au je, nilifanya dhambi kwa kujinyenyekeza ili ninyi mwinuliwe, kwa sababu nili-

10:17, 18 *Angalia Nyongeza A5. **11:2** *Tnn., "bidii ya Mungu." #Au "safi kiadili." **11:3** *Au "usafi wa kiadili."

SURA YA 10

a Yer 9:24
1Ko 1:31

b Lu 18:10-14

c 1Ko 4:5
2Ti 2:15

SURA YA 11

d Mk 2:19
Efe 5:23
Ufu 21:2, 9

e Mwa 3:4, 5
Yoh 8:44

f 1Ti 6:3-5
Ebr 13:9
2Pe 3:17

g Gal 1:7, 8

h 2Ko 11:23

i 2Ko 10:10

Safu ya 2

a Mdo 18:3
1Ko 9:18

b Flp 4:10

c Flp 4:15, 16

d 1Th 2:9

e 1Ko 9:14, 15

f 1Ko 9:11, 12

g Ro 16:17, 18
2Pe 2:1

h Gal 1:8
2Th 2:9

i Mt 16:27
Flp 3:18, 19
2Ti 4:14

watangazia habari njema ya Mungu kwa furaha bila gharama?^a **8** Niliyanyang'anya* makutaniko mengine kwa kupokea vitu[#] kutoka kwao ili niwahudumie ninyi.^b **9** Na bado, nilipokuwa pamoja nanyi na nikapatwa na uhitaji, sikuwa mzigo kwa mtu yeyote, kwa maana ndugu waliotoka Makedonia walinipatia mahitaji yangu kwa wingi.^c Ndiyo, katika kila njia sikutaka kuwa mzigo kwenu nami nitaendelea kufanya hivyo.^d **10** Kwa hakika ikiwa kweli ya Kristo imo ndani yangu, sitaacha kujisifu^e katika maeneo ya Akaya. **11** Kwa sababu gani? Je, ni kwa sababu siwapendi? Mungu anajua ninawapenda.

12 Lakini nitaendelea kufanya kile ninachofanya,^f ili niondoe kisingizio cha wale wanaotafuta sababu ya kuonekana* kuwa sawa na sisi katika mambo ambayo[#] wana-jisifia. **13** Kwa maana watu wa namna hiyo ni mitume wa uwongo, wafanyakazi wadanganyifu, wanaojifanya kuwa mitume wa Kristo.^g **14** Na si ajabu, kwa maana Shetani mwenyewe huendelea kujifanya kuwa malaika wa nuru.^h **15** Kwa hiyo si ajabu kwamba wahudumu wake pia huendelea kujifanya kuwa wahudumu wa uadilifu. Lakini mwisho wao utakuwa kulingana na matendo yao.ⁱ

16 Ninasema tena: Mtu yeyote asifikiri kwamba mimi sina akili. Lakini hata mkifikiri hivyo, basi mnikubali kama mtu asiye na akili, ili mimi

11:8 *Au "Niliyapora." #Au "msaada." **11:12** *Au "kisingizio cha." #Au "cheo ambacho."

pia nijisifu kidogo. **17** Hili ndilo ninalosema sasa, si kwa kufuata kielelezo cha Bwana, bali kama mtu asiye na akili, kwa ujasiri wa kujisifu. **18** Kwa kuwa wengi wanajisifu kulingana na mwili,* mimi pia nitajisifu. **19** Kwa kuwa ninyi mna "akili" sana, mnakubaliana kwa furaha na watu wasio na akili. **20** Kwa kweli, mnakubaliana na yeyote anayefanya kuwa watumwa, yeyote anayemeza mali yenu, yeyote anayenyakua kile mlichicho nacho, yeyote anayejitukuza juu yenu, na yeyote anayewapiga usoni.

21 Ninasema hili kwa aibu yetu, kwa sababu huenda ikaonekana tumetenda kwa udhaifu.

Lakini ikiwa wengine wanatenda kwa ujasiri—ninazungumza kama mtu asiye na akili—mimi pia ninatenda kwa ujasiri. **22** Je, wao ni Waebrania? Mimi pia.^a Je, wao ni Waisraeli? Mimi pia. Je, wao ni uzao wa* Abrahamu? Mimi pia.^b **23** Je, wao ni wahudumu wa Kristo? Ninajibu kama mwendawazimu, mimi ni mhudumu kwa njia kubwa hata zaidi: Nimefanya kazi nyingi zaidi,^c nimefungwa gerezani mara nyingi zaidi,^d nimepigwa mara nyingi sana, na kukaribia kufa mara nyingi.^e **24** Mara tano nilipigwa na Wayahudi viboko 40 kaso-ro kimoja,^f **25** mara tatu nilipigwa kwa fimbo,^g mara moja nilipigwa mawe,^h mara tatu nilivunjikiwa na meli,ⁱ usiku mmoja na mchana mmoja nimekaa baharini; **26** mara

11:18 *Yaani, kwa maoni ya wanadamu.
11:22 *Tnn., "mbegu ya."

SURA YA 11

a Mdo 22:3

b Ro 11:1
Flp 3:4, 5c Ro 11:13
1Ko 15:10

d Mdo 16:23, 24

e Mdo 9:15, 16
2Ko 6:4, 5
1Pe 2:20, 21

f Kum 25:3

g Mdo 16:22

h Mdo 14:19

i Mdo 27:41

Safu ya 2

a Mdo 20:3
Mdo 23:10

b Mdo 14:5, 6

c Mdo 13:50

d Mdo 20:31

e 1Ko 4:11

f 2Ko 6:4, 5

g 2Ko 2:4
Kol 2:1

h Mdo 9:24, 25

SURA YA 12

i Mdo 2:17

j Mdo 22:17, 18

nyingi katika safari, hatari za kutokana na mito, hatari za kutokana na wezi, hatari za kutokana na watu wangu mwenyewe,^a hatari za kutokana na mataifa,^b hatari jijini,^c hatari nyikani, hatari baharini, hatari kati ya ndugu wa uwongo, **27** kwa kazi ngumu na yenye kutaabisha, mara nyingi kukosa usingizi usiku,^d njaa na kiu,^e kukosa chakula mara nyingi,^f na pia baridi na kukosa mavazi.*

28 Zaidi ya mambo hayo ya nje, pia kuna jambo linalonipata siku kwa siku:* kuhangaikia makutaniko yote.^g **29** Ni nani aliye dhaifu, nami si dhaifu? Ni nani amekwazika, nami sina hasira?

30 Ikiwa ni lazima nijisifu, nitajisifu kuhusu mambo yanayoonyesha udhaifu wangu. **31** Mungu na Baba ya Bwana Yesu, Yule anayestahili kusifiwa milele, anajua sise mi uwongo. **32** Huko Damasko gavana aliye chini ya Areta mfalme alikuwa akilinda jiji la Wadamasko ili kunikamata, **33** lakini nilishushwa katika kapu kupitia dirisha kwenye ukuta wa jiji,^h nami nikai-ponyoka mikono yake.

12 Lazima nijisifu. Hakuna faida, lakini nitaenda kwenye maonoⁱ ya miujiza na ufunuo wa Bwana.^j **2** Ninamjua mtu fulani katika muungano na Kristo, ambaye miaka 14 iliyopita—kama ni katika mwili au nje ya mwili, sijui; Mungu anajua—alinyakuliwa mpaka kwenye mbingu

11:27 *Tnn., "katika uchi." 11:28 *Au "kuna mambo yanayonikaza kila siku kuhusu."

ya tatu. **3** Ndiyo, ninamjua mtu kama huyo—iwe ni katika mwili au bila mwili, mimi sijui; Mungu anajua— **4** ambaye alinyakuliwa kuingia katika paradiso na kusikia maneno yasiyoweza kutamkwa na ambayo si halali kwa mtu kuyasema. **5** Nitajisifu kuhusu mtu wa namna hiyo, lakini sitajisifu kuhusu mimi mwenyewe isipokuwa kuhusu udhaifu wangu. **6** Kwa maana hata nikitaka kujisifu, sitakuwa mtu asiye na akili, kwa kuwa nitasema ukweli. Lakini sitaki kufanya hivyo, ili yeyote asinisifu zaidi ya yale anayoona kwangu au kusikia kutoka kwangu, **7** kwa sababu tu ya kupokea maono hayo ya ajabu.

Ili nisijiinue mno, nilipewa mwiba katika mwili,^a malaika wa Shetani, aendeleo kunipiga kofi,* ili nisijiinue kupita kiasi. **8** Mara tatu nilimwomba Bwana kuhusu jambo hili, kwamba aniondolee. **9** Lakini akaniambia: “Fadhili zangu zisizostahiliwa zinakutosha, kwa kuwa nguvu zangu zinakamilika katika udhaifu.”^b Kwa furaha zaidi, basi, nitajisifu kuhusu udhaifu wangu, ili nguvu za Kristo zibaki juu yangu kama hema. **10** Basi ninapendezwa na udhaifu, na matusi, na nyakati za uhitaji, na mateso na shida, kwa ajili ya Kristo. Kwa maana ninapokuwa dhaifu, ndipo ninapokuwa na nguvu.^c

11 Nimekuwa mtu asiye na akili. Mlinilazimisha kuwa hivyo, kwa sababu ninyi mlipaswa kunipendekeza. Kwa maa-

12:7 *Au “kunipiga.”

SURA YA 12

a Gal 4:13

b Isa 40:29

c Flp 4:13

Safu ya 2

a 2Ko 11:23

b 2Ko 6:4

c Mdo 14:3
Mdo 15:12
Ro 15:18, 19

d 1Ko 9:11, 12
2Ko 11:9

e Mdo 20:33

f 1Ko 4:14

g 2Ko 1:6
Kol 1:24
1Th 2:8
Ebr 13:17

h 2Ko 11:9

i 2Ko 8:6

na hata katika jambo moja si kuwa mdogo kuliko mitume wenu walio bora sana, hata kama mimi si kitu.^a **12** Kwa kweli, ishara za mtume zilitokezwa kati yenu kwa uvumilivu mkubwa,^b na kwa ishara na mambo ya ajabu* na mateendo yenye nguvu.^c **13** Ni kwa njia gani mlíkosa kupendelewa kuliko makutaniko mengine, isipokuwa kwamba mimi mwenyewe sikuwa mzigo kwenu?^d Mnisamehe kosa hili kwa fadhili.

14 Tazama! Hii ni mara ya tatu niliyo tayari kuja kwenu, nami sitakuwa mzigo. Kwa kuwa ninawatafuta ninyi, si mali zenu;^e kwa maana watoto^f hawatarajiwi kuweka aki-ba kwa ajili ya wazazi wao, bali wazazi kwa ajili ya watoto wao. **15** Kwa upande wangu, nitatumia kwa furaha zaidi na kutumiwa kabisa kwa ajili yenu.^g Kama nikiwapenda ninyi sana, je, mimi nipendwe kidogo? **16** Lakini hata iwe-je, mimi sikuwa mzigo kwenu.^h Hata hivyo mnasema, nilikuwa “mjanja” na niliwashika “kwa ujanja.” **17** Sikujifaidi kutoka kwenu kupitia yeyote kati ya wale niliowatuma kwenu, sivyo? **18** Nilimhimi-za Tito na nikamtuma yule ndugu pamoja naye. Je, kweli Tito alijifaidi kutoka kwenu?ⁱ Tulitembea katika roho ileile, sivyo? Katika hatua zilezile, sivyo?

19 Je, mnafikiri kwamba muda huu wote tumekuwa tukijitetea kwenu? Tunazungumza mbele za Mungu katika muungano na Kristo.

12:12 *Au “miujiza.” 12:15 *Au “nafsi zenu.”

Lakini wapendwa, yote tunayofanya ni kwa ajili ya kuwajenga. **20** Kwa maana ninaogopa kwamba huenda nitakapofika, sitawakuta mkiwa kama ninavyotaka nami sitakuwa kama mnavyotaka, badala yake, huenda kuna mizozo, wivu, milipuko ya hasira, migawanyiko, masengenyo, minong'ono,* kujivuna kwa kiburi, na machafuko. **21** Labda nitakapokuja tena, huenda Mungu wangu akaninyenyekeza mbele yenu, nami niwaombolezee wengi kati ya wale ambao mwanzoni walitenda dhambi lakini hawajatubu unajisi wao na uasherati* na mwenendo mpotovu# ambao wametenda.

13 Hii ni mara ya tatu ambayo ninakuja kweni. "Kila jambo linapaswa kuthibitishwa kwa ushahidi wa* mashahidi wawili au watatu."^a **2** Ingawa sipo sasa, ni kana kwamba nipo kwa mara ya pili, nami ninatoa onyo mape-ma kwa wale waliotenda dhambi mwanzoni na kwa wengine wote, kwamba ikiwa nitakuja tena sitawahurumia, **3** kwa kuwa mnatafuta uthibitisho kwamba Kristo, ambaye si dhaifu kuwaelekea ninyi bali ni mwenye nguvu kati yenu, kwa kweli anazungumza kupitia mimi. **4** Ni kweli kwamba aliuawa kwenye mti kwa sababu ya udhaifu, lakini yuko hai kwa sababu ya nguvu za Mungu.^b Ni kwe-

12:20 *Au "umbeya." 12:21 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki, *a-sel'gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 13:1 *Tnn., "kinywa cha."

SURA YA 13

a Kum 19:15
Mt 18:16

b Ro 6:4
1Pe 3:18

Safu ya 2

a 2Ti 2:11, 12

b 1Ko 6:14

c 1Ko 11:28
Gal 6:4

d 1Ko 4:21

e 2Ko 1:3, 4

f Flp 2:2

g 1Th 5:13
Yak 3:17
1Pe 3:11
2Pe 3:14

h 1Ko 14:33

li kwamba sisi pia ni dhaifu pamoja naye, lakini tutaishi pamoja naye^a kwa sababu ya nguvu za Mungu kuwaelekea ninyi.^b

5 Endeeleni kujijaribu kama mko katika imani, endeeleni kuthibitisha jinsi ninyi wenyewe mlivyo.^c Au je, hamtambui kwamba Yesu Kristo yumo katika muungano pamoja nanyi? Isipokuwa muwe mmekataliwa. **6** Kwa kweli ninatumaini mtatambua kwamba hatujakataliwa.

7 Basi tunasali kwa Mungu kwamba msifanye kosa, si ili sisi tuonekane kuwa waliokubaliwa, bali mfanye yaliyo mema, hata tukionekana kwamba tumekataliwa. **8** Kwa maana hatuwezi kufanya jambo lolote kinyume cha kweli, bali kwa ajili ya kweli. **9** Hakika sisi hushangilia kila mara tunapokuwa dhai-fu lakini ninyi mna nguvu. Nasi tunasali kwamba mrekebishwe upya. **10** Hiyo ndiyo sababu ninaandika mambo haya nikiwa sipo, ili nitakapokuja, nisiwe mkali katika kutumia mamlaka ambayo Bwana alinipa,^d ili kujenga na si kubomoa.

11 Mwishowe, akina ndugu, endeeleni kushangilia, kurekebishwa upya, kufarijiwa,^e kufikiri kwa upatano,^f kui-shi kwa amani;^g na Mungu wa upendo na amani^h atakuwa pamoja nanyi. **12** Salimiane-ni kwa busu takatifu. **13** Wakatatifu wote wanawatumia salamu zao.

14 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana Yesu Kristo na upendo wa Mungu na ushirika katika roho takatifu ziwe pamoja nanyi nyote.

KWA
WAGALATIA

YALIYOMO

- | | |
|---|--|
| <p>1 Salamu (1-5)
Hakuna habari njema nyingine (6-9)
Habari njema aliyohubiri Paulo inatoka kwa Mungu (10-12)
Jinsi Paulo alivyogeuka na kazi yake ya mwanzoni (13-24)</p> <p>2 Paulo akutana na mitume huko Yerusalemu (1-10)
Paulo amrekebisha Petro (Kefa) (11-14)
Kutangazwa kuwa waadilifu kupitia imani tu (15-21)</p> <p>3 Tofauti kati ya matendo ya Sheria na imani (1-14)
Mwadilifu ataishi kupitia imani (11)
Ahadi kwa Abrahamu haikuwa kupitia Sheria (15-18)
Kristo, uzao wa Abrahamu (16)
Chanzo na kusudi la Sheria (19-25)</p> | <p>Wana wa Mungu kupitia imani (26-29)
Wazao wa Abrahamu, wale walio wa Kristo (29)</p> <p>4 Si watumwa tena, bali ni wana (1-7)
Paulo awahangaikia Wagalatia (8-20)
Hagari na Sara: maagano mawili (21-31)
Yerusalemu lililo juu, mama yetu, liko huru (26)</p> <p>5 Uhuru wa Kikristo (1-15)
Kutembea kwa roho (16-26)
Matendo ya mwili (19-21)
Tunda la roho (22, 23)</p> <p>6 Kubebeana mizigo (1-10)
Kuvuna ulichopanda (7, 8)
Kutahiriwa si muhimu (11-16)
Kiumbe kipya (15)
Umalizio (17, 18)</p> |
|---|--|

1 Paulo, mtume, si kutokana na wanadamu wala kupitia mwanadamu, bali kupitia Yesu Kristo^a na Mungu Baba,^b aliyemfufua kutoka kwa wafu, **2** na ndugu wote walio pamoja nami, kwa makutaniko ya Galatia:

3 Na muwe na fadhili zizozostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo. **4** Alijitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zetu^c ili atuokoe kutoka katika mfumo huu mwovu wa mambo,^d kulingana na mapenzi ya Mungu na Baba yetu,^e **5** na awe na utukufu milele na milele. Amina.

6 Ninashangaa kwamba mna-

1:4 * Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo."

SURA YA 1

a Mdo 9:15
Mdo 26:15, 16

b Mdo 22:14, 15

c 1Yo 2:1, 2

d Yoh 15:19

e 1Ti 2:3, 4

Safu ya 2

a 2Ko 11:3, 4
Gal 5:7

b Gal 5:10

geuzwa* upesi kutoka kwa Yule aliyewaita kwa fadhili zizozostahiliwa za Kristo nanyi mnaenda kwenye habari njema ya aina nyingine.^a **7** Si kwamba kuna habari njema nyingine; lakini kuna watu fulani wanaowataabisha ninyi^b na kutaka kupotosha habari njema kuhusu Kristo. **8** Hata hivyo, ikiwa sisi au malaika kutoka mbinguni tungewatangazia kuwa habari njema jambo tofauti na habari njema tuliyowatangazia, mtu huyo na alaaniwe. **9** Kama tulivyosema awali, sasa ninasema tena, Yeyote anayewatangazia kuwa habari njema jambo tofauti na lile mlilopokea, na alaaniwe.

1:6 * Au "mnaondolewa."

10 Kwa kweli, je, sasa ninajaribu kuwashawishi wanadamu au Mungu? Au je, ninajaribu kuwapendeza wanadamu? Kama bado ningekuwa ninawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo. **11** Akina ndugu, ningependa mjue kwamba habari njema niliyowatangazia haitokani na wanadamu;^a **12** kwa kuwa sikuipokea kutoka kwa mwanadamu, wala sikufundishwa, bali ilikuwa kupitia ufunuo wa Yesu Kristo.

13 Bila shaka, mlisikia kuhusu mwenendo wangu wa zamani katika dini ya Kiyahudi,^b kwamba niliendelea kuli-tesa sana* kutaniko la Mungu na kuliangamiza;^c **14** nami nilikuwa nikifanya maendeleo makubwa katika dini ya Kiyahudi kuliko watu wengi wa umri wangu katika taifa langu, kwa maana nilikuwa na bidii zaidi kwa ajili ya mapokeo ya baba zangu.^d **15** Lakini Mungu, aliyenitenga tangu tumbo la uzazi la mama yangu na kuniita kupitia fadhili zake zisizostahiliwa,^e alipoonavema **16** kumfunua Mwana wake kupitia kwangu, ili niyangazie mataifa habari njema kumhusu,^f sikushauriana papo hapo na mwanadamu yeyote;* **17** wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa wale waliokuwa mitume kabla yangu, bali niliendelea Arabia, kisha nikarudi Damasko.^g

18 Miaka mitatu baadaye, nilipanda kwenda Yerusalemu^h kumtembelea Kefa,*ⁱ nami nikakaa pamoja naye siku 15. **19** Lakini sikuwaona

1:13 *Tnn., "mpaka hatua inayozidi mno." 1:16 *Tnn., "na mwili na damu." 1:18 *Pia anaitwa Petro.

SURA YA 1

a 1Th 2:13

b Mdo 23:6

c Mdo 8:3
Mdo 9:1, 2
Mdo 22:4
Mdo 26:9-11d Mdo 22:3
Flp 3:4-6

e 1Ko 15:10

f Mdo 9:15
Ro 11:13

g Mdo 9:19

h Mdo 9:26

i Yoh 1:42
1Ko 15:5

Safu ya 2

a Mt 13:55
Mdo 12:17

b Mdo 9:29, 30

c Gal 1:13

d Mdo 8:3

SURA YA 2

e Mdo 9:27

f Mdo 15:1, 2

g 2Ko 2:13

h Mdo 16:3

i Mdo 15:1, 24

j 2Ko 3:17
Gal 5:1

k Gal 4:9

l Gal 2:14

wale mitume wengine, isipokuwa Yakobo^a ndugu wa Bwana. **20** Basi kuhusu mambo ninayowaandikia, ninawahakikishia mbele za Mungu kwaamba sisemi uwongo.

21 Baada ya hapo nikaenda katika maeneo ya Siria na Kilikia.^b **22** Lakini mimi binafsi sikujulikana kwa makutani-ko ya Yudea yaliyokuwa katika muungano na Kristo. **23** Walikuwa tu wakisikia: "Yule mtu ambaye alitutesa^c hapo zamani sasa anatangaza habari njema kuhusu imani ambayo hapo zamani aliiangamiza."^d **24** Basi wakaanza kumtukuza Mungu kwa sababu yangu.

2 Baada ya miaka 14 nilipanda tena kwenda Yerusalemu pamoja na Barnaba,^e na Tito pia.^f **2** Lakini nili-enda kutokana na ufunuo, nami nikawajulisha habari njema ambayo ninahubiri kati ya mataifa. Hata hivyo, nilifanya hivyo faraghani, mbele ya wanaume walioheshimiwa sana, ili kuhakikisha kwaamba sikuwa ninakimbia bure au sikuwa nimekimbia bure. **3** Hata hivyo, hata Tito,^g aliyekuwa pamoja nami, haku-lazimishwa kutahiririwa,^h ingawa alikuwa Mgiriki. **4** Lakini jambo hilo lilitokea kwa sababu ya akina ndugu wa uwongo walioingizwa kimyakimya,ⁱ walioingia kisirisiri ili kupeleleza uhuru^j tunaofurahia katika muungano na Kristo Yesu, ili watafanye kuwa watumwa kabisa;^k **5** hatukukubaliana nao wala kujitiisha kwao,^l hapano, hata kwa muda mfupi,* ili kweli ya habari njema iendelee kuwa pamoja nanyi.

2:5 *Tnn., "kwa saa moja."

6 Lakini kuhusu wale walioonekana kuwa muhimu^a—vyovyote walivyokuwa hapo awali sioni tofauti, kwa maana Mungu haangalii sura ya nje—watu hao walioheshimiwa sana hawakuniongezea kitu chochote kipya. 7 Badala yake, walipoona kwamba nilikuwa nimekabidhiwa habari njema kwa ajili ya wale wasiotahiriwa,^b kama vile Petro alivyokabidhiwa kwa ajili ya wale waliotahiriwa— 8 kwa maana yule aliyemtia Petro nguvu kwa ajili ya utume kwa wale waliotahiriwa, alinitia nguvu mimi pia kwa ajili ya watu wa mataifa^c— 9 nao walipotambua fadhili zisizostahiliwa nilizopewa,^d Yakobo^e na Kefa* na Yohana, ambao walionekana kuwa nguzo, walinipa mimi na Barnaba^f mkono wa kulia wa kushirikiana,^g ili sisi twe nde kwa mataifa, nao wae nde kwa watu waliotahiriwa. 10 Walituomba tuwakumbuke maskini, nami nimejitahidi sana kufanya jambo hilo.^g

11 Hata hivyo, Kefa*^h alipokuja Antiokia,ⁱ nilimpinga^h uso kwa uso, kwa sababu kwa hakika alikuwa amekosea.^h 12 Kwa maana kabla ya watu fulani kutoka kwa Yakobo^j kufika, alikuwa akila chakula pamoja na watu wa mataifa;^k lakini walipofika, akaacha kufanya hivyo, akajitenga kwa kuwaogopa wale waliotahiriwa.^l 13 Wayahudi wengine pia wakajiunga naye katika unafiki huo, hivi kwamba hata wakamshawishi Barnaba katika unafiki wao. 14 Laki-

2:9, 11, 14 *Pia anaitwa Petro. 2:9 #Au "ushirikiano." 2:11 #Au "nilimkabili."
^aAu "alikuwa na hatia."

SURA YA 2

a Gal 2:9

b Mdo 22:21
Ro 11:13
1Ti 2:7

c Mdo 9:15

d Efe 3:8

e Mdo 15:13

f Mdo 13:2
Mdo 15:25g Mdo 11:29, 30
1Ko 16:1

h Yoh 1:42

i Mdo 11:25, 26
Mdo 15:35

j Mdo 12:17

k Mdo 10:26, 28
Mdo 11:2, 3

l Mdo 21:20, 21

Safu ya 2

a Mdo 10:34, 35

b Mdo 15:10
Mdo 15:28, 29c Ro 1:17
Yak 2:23d Mdo 13:39
Ro 5:17
1Ko 6:11

e Ro 3:20-22

f Ro 7:9

g Ro 6:6
Gal 5:24

h 1Pe 4:1, 2

i 2Ko 5:15

ni nilipoona kwamba hawakuwa wakitembea kwa unyoo-fu kulingana na kweli ya habari njema,^a nilimwambia Kefa* mbele yao wote: "Ikiwa wewe, ingawa ni Myahudi unaishi kama mataifa wanavyoishi, na si kama Wayahudi wanavyoishi, unawezaje kuwalazimisha watu wa mataifa waishi kulingana na mazoea ya Kiyahudi?"^b

15 Sisi tulio Wayahudi kwa kuzaliwa, na si watenda dhambi kutoka kwa mataifa, 16 tunatambua kwamba mtu hutangazwa kuwa mwadilifu, si kupitia matendo ya sheria, bali kupitia tu imani^c katika Yesu Kristo.^d Basi sisi tumeweka imani yetu katika Kristo Yesu, ili tutangazwe kuwa waadilifu kupitia imani katika Kristo bali si kupitia matendo ya sheria, kwa maana hakuna mtu yeyote atakayetangazwa* kuwa mwadilifu kupitia matendo ya sheria.^e 17 Sasa ikiwa sisi pia tumepatikana kuwa watenda dhambi tulipokuwa tukitafuta kutangazwa kuwa waadilifu kupitia Kristo, basi je, Kristo ni mhudumu wa dhambi? La hash! 18 Ikiwa ninayajenga tena mambo ambayo wakati mmoja niliyabomoa, ninaonyesha kwamba mimi ni mkosaji. 19 Kwa maana kupitia sheria nilikufa kuielekea sheria,^f ili niwe hai kumwelekea Mungu. 20 Mimi nimetundikwa mtini pamoja na Kristo.^g Si mimi tena niliye hai,^h bali ni Kristo anayeishi katika muungano na mimi. Kwa kweli, uhai ninaoishi sasa katika mwili ninaishi kwa imani katika Mwana wa Mungu,ⁱ aliye-

2:16 *Tnn., "mwili utakaotangazwa."

nipenda na kujitoa mwenyewe kwa ajili yangu.^a **21** Mimi sizikatai* fadhili zisizostahiliwa za Mungu,^b kwa maana ikiwa uadilifu ni kupitia sheria, kwa kweli Kristo alikufa bure.^c

3 Enyi Wagalatia wasio na akili! Ni nani aliyewaleta chini ya uvutano huu mwovu,^d ninyi mliofafanuliwa waziwazi jinsi Yesu Kristo alivyotundikwa mtini?^e **2** Ninataka kuwauliza* jambo hili moja: Je, mlipokea roho kupitia mateendo ya sheria au kwa sababu ya kuamini mambo mliyosikia?^f **3** Je, ninyi hamna akili kabisa? Baada ya kuanza mwendo wa kiroho,* je, mnamalizia katika mwendo wa kimwili?^g **4** Je, mli-patwa na mateso mengi sana bila sababu? Ikiwa kwa kweli ilikuwa bila sababu. **5** Kwa hiyo, je, yule anayewapa ninyi roho na kufanya matendo yenye nguvu^h kati yenu, anayafanya kwa sababu ya mateendo ya sheria au kwa sababu mnaamini mambo mliyosikia? **6** Kama vile Abrahamu “alivyokuwa na imani katika Yehova,* na ikahesabiwa kwake kuwa ni uadilifu.”ⁱ

7 Bila shaka mnajua kwamba wale wanaoshikamana na imani ni wana wa Abrahamu.^j **8** Kwa hiyo, andiko likitangulia kuona kwamba Mungu atawatangaza watu wa mataifa kuwa waadilifu kupitia imani, lilitangaza habari njema mwanzoni kwa Abrahamu, yaani: “Kupitia kwako mataifa yote yatabarikiwa.”^k

2:21 *Au “sizitupi.” 3:2 *Tnn., “kujifunza kutoka kwenu.” 3:3 *Tnn., “kuanza katika roho.” #Tnn., “mnakamilishwa katika mwili.” 3:6 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 2

a 1Ti 2:5, 6

b Yoh 1:17

c Gal 3:21
Ebr 7:11

SURA YA 3

d Gal 5:7

e 1Ko 1:23

f Efe 1:13

g Gal 4:9,10

h 1Ko 12:8-10

i Mwa 15:6
Ro 4:3
Yak 2:23

j Ro 4:11, 12

k Mwa 12:3
Mwa 18:18

Safu ya 2

a Ro 4:16, 17

b Kum 27:26
Mdo 15:10
Yak 2:10

c Gal 2:15, 16

d Hab 2:4
Ro 1:17
Ebr 10:38e Law 18:5
Kum 30:16
Ro 10:5

f 1Ko 7:23

g Mt 26:27, 28
Ebr 9:15h Kum 21:23
Mdo 5:30

i Efe 2:15, 16

j Yoe 2:28

k Mwa 12:1-3
Mwa 12:7
Mwa 13:14, 15
Mwa 17:7
Mwa 22:17, 18
Mwa 24:7

l Mt 1:17

9 Basi wale wanaoshikamana na imani wanabarikiwa pamoja na Abrahamu, aliyekuwa na imani.^a

10 Wote wanaotegemea matendo ya sheria wako chini ya laana, kwa maana imeandikwa: “Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika mambo yote yaliyoandikwa katika kitabu cha kukunjwa cha Sheria kwa kuyatenda.”^b **11** Isitoshe, ni wazi kwamba kupitia sheria hakuna mtu atakayatangazwa kuwa mwadilifu mbele za Mungu,^c kwa maana “mwadilifu ataishi kupitia imani.”^d **12** Sasa Sheria haitegemei imani. Badala yake, “yeyote anayefanya mambo hayo ataishi kupitia mambo hayo.”^e **13** Kristo alitununa,^f akatuweka huru^g kutoka katika laana ya Sheria akawa laana badala yetu, kwa sababu imeandikwa: “Amelaaniwa kila mtu aliyetundikwa kwenye mti.”^h **14** Ilikuwa hivyo ili baraka ya Abrahamu ije kwa mataifa kupitia Kristo Yesu,ⁱ ili tuipokee roho iliyoahidiwa/ kupitia imani yetu.

15 Akina ndugu, ninazungumza kwa kutumia mfano wa mwanadamu: Agano lina-pohalalishwa, hata kama ni kupitia mwanadamu, hakuna mtu anayelifuta au kuliongezea jambo lolote. **16** Sasa ahadi zilitolewa kwa Abrahamu na kwa uzao wake.^{*k} Haisemi, “na kwa wazao wako,”# kana kwamba ni wengi. Badala yake, inasema, “na kwa uzao wako,”[^] kana kwamba ni kwa mmoja, ambaye ni Kristo.^l **17** Isitoshe, ninasema hivi: Sheria iliyotokezwa

3:16 *Tnn., “mbegu yake.” #Tnn., “mbegu zako.” ^Tnn., “mbegu yako.”

miaka 430 baadaye,^a haivunji agano lililofanywa na Mungu mwanzoni, na haifuti ahadi. **18** Kwa maana ikiwa urithi unategemea sheria, hautegemei tena ahadi; lakini Mungu amempa Abrahamu urithi kwa fadhili kupitia ahadi.^b

19 Basi, kwa nini Sheria? Iiongezwa ili kufanya makosa yawe wazi,^c mpaka ufike ule uzao^{*d} ambao ulikuwa umepelewa ahadi; na ilipitishwa kupitia malaika^e kwa mkono wa mpatanishi.^f **20** Sasa hakuna mpatanishi wakati mtu mmoja tu ndiye anayehusika, lakini Mungu ni mmoja tu. **21** Kwa hiyo, je, Sheria inapinga ahadi za Mungu? La hasha! Kwa maana ikiwa kungekuwa na sheria inayoweza kuleta uhai, kwa kweli uadilifu ungekuwa kupitia sheria. **22** Lakini Andiko liliyafunga mambo yote katika kifungo cha dhambi, ili ahadi inayotokana na imani katika Yesu Kristo ipewe wale wanaoamini.*

23 Hata hivyo, kabla ya imani kufika, tulikuwa tukilindwa chini ya sheria, tukiwekwa kifungoni, tukiitazamia imani iliyokusudiwa kufunuliwa.^g **24** Basi Sheria imekuwa mtunzaji* wetu ikituongoza kwa Kristo,^h ili tutangazwe kuwa waadilifu kupitia imani.ⁱ **25** Lakini sasa kwa kuwa imani imefika,^j hatuko tena chini ya mtunzaji.*^k

26 Kwa kweli, ninyi nyote ni wana wa Mungu^l kupitia imani yenu katika Kristo Yesu.^m **27** Kwa maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.ⁿ **28** Haku-

3:19 *Tnn., "ile mbegu." 3:22 *Au "wanaonyesha imani." 3:24, 25 *Au "mfundishaji; mlezi."

SURA YA 3

a Kut 12:40, 41

b Mwa 22:17

c Ro 3:20

d Yoh 1:29
Ro 10:4e Mdo 7:38, 53
Ebr 2:2f Kut 20:19
Kum 5:5
Yoh 1:17

g Ro 10:4

h Mt 5:17

i Mdo 13:39
Ro 5:1
Ro 8:33

j Kol 2:17

k Ebr 8:6

l Ro 8:14

m Yoh 1:12

n Ro 13:14
Efe 4:24

Safu ya 2

a Ro 10:12

b 1Ko 12:13
Kol 3:10, 11c Mdo 2:17
1Pe 3:7

d Yoh 17:20, 21

e Ro 9:7, 8

f Ro 8:17

g Mwa 22:18

SURA YA 4

h Kol 2:8

i Yoh 1:14
Ebr 2:14

j Mt 5:17

k 1Ko 7:23
Gal 3:13l Yoh 1:12
Ro 8:23

m Yoh 14:26

n Ro 5:5

o Ro 8:15

p Ro 8:17
Gal 3:29
Efe 1:13, 14

na Myahudi wala Mgiriki,^a hakuna mtumwa wala mtu huru,^b hakuna mwanamume wala mwanamke,^c kwa maana ninyi nyote ni kitu kimoja katika muungano na Kristo Yesu.^d **29** Isitoshe, ikiwa ninyi ni wa Kristo, ninyi kwa kweli ni uzao wa* Abrahamu,^e warithi^f kuhusiana na ahadi.^g

4 Basi ninasema kwamba mrithi akiwa bado mto- to mdo, hayuko tofauti na mtumwa, ingawa ndiye bwana wa vitu vyote, **2** bali yuko chini ya watunzaji na wasimamizi mpaka siku iliyopangwa mapema na baba yake. **3** Vivyo hivyo, sisi pia tulipokuwa watoto, tulikuwa watumwa wa mambo ya msingi ya ulimwengu.^h **4** Lakini wakati kamili ulipofika, Mungu alituma Mwana wake, aliyezaliwa na mwanamkeⁱ na pia alikuwa chini ya sheria,^j **5** ili awaachilie huru kwa kuwanunua wale walio chini ya sheria,^k ili sisi tufanywe kuwa wana.^l

6 Sasa kwa sababu ninyi ni wana, Mungu ametuma roho^m ya Mwana wake ndani ya mioyo yetu,ⁿ nayo hupaza sauti: "Abba,* Baba!"^o **7** Kwa hiyo, wewe si mtumwa tena bali ni mwana; na ikiwa ni mwana, basi wewe pia ni mrithi kupitia Mungu.^p

8 Hata hivyo, wakati hamkumjua Mungu, mlikuwa watumwa wa miungu ya uongo.* **9** Lakini sasa kwa kuwa mmemjua Mungu au, kwamba sasa Mungu amewajua ninyi, kwa nini mnarudi

3:29 *Tnn., "mbegu ya." 4:6 *Neno la Kiebrania au Kiaramu linalomaanisha "Ee Baba!" 4:8 *Tnn., "ile ambayo kwa kweli si miungu."

tena kwenye mambo ya msingi yaliyo dhaifu^a na yasiyo na maana na kutaka kuyatumikia tena?^b **10** Mnashika kwa uangalifu sana siku na miezi^c na majira na miaka. **11** Ninaogopa kwa ajili yenu, isiwe kwamba nimepoteza jitihada zangu kwenu.

12 Ninawaomba akina ndugu, iweni kama nilivyo, kwa sababu mimi pia nilikuwa kama mlivyo.^d Hamkunikosea. **13** Lakini mnajua ni kwa sababu ya ugonjwa wa kimwili kwamba nilipata nafasi yangu ya kwanza ya kuwatangazia habari njema. **14** Na ingawa hali yangu ya kimwili ilikuwa jaribu kwenu, hamkunite ndea kwa dharau au kunichukia;* bali mlinipokea kama malaika wa Mungu, kama Kristo Yesu. **15** Furaha mliyokuwa nayo iko wapi? Kwa maana ninawatolea ushahidi kwamba, kama ingewezekana, mngayang'oa macho yenu na kunipa.^e **16** Hivyo basi, je, nimekuwa adui yenu kwa sababu ninawaambia ukweli? **17** Wanawatafuta kwa bidii ili muwafuate, bali si kwa kusudi zuri; wanataka kuwatenanisha nami, ili muwafuate wao kwa bidii. **18** Hata hivyo, ni vema sikuzote kwa mtu kuwatafuta ninyi kwa bidii kwa kusudi zuri bali si wakati tu ninapokuwa pamoja nanyi, **19** watoto wangu wadogo,^f ambao tena nina uchungu wa kuwazaa mpaka Kristo atakapofanyizwa* ndani yenu. **20** Ninatamani ningekuwa pamoja nanyi sasa hivi na kuzungumza kwa njia to-

4:14 *Au "kunitemea mate." 4:19 *Au "atakapoubwa."

SURA YA 4

a Ro 8:3
Ebr 7:18,19

b Kol 2:20-22

c Kol 2:16

d Gal 1:14

e Mdo 23:5
Gal 6:11

f 1Ko 4:15
1Th 2:11
Flm 10

Safu ya 2

a Mwa 16:15

b Mwa 21:2,3

c Mwa 16:1,2

d Mwa 17:15,16

e Kut 19:20
Kut 24:12

f Kut 19:18

g Isa 54:1

h Ro 9:8
Gal 3:29

i Mwa 21:9

j Gal 5:11
2Ti 3:12

fauti, kwa sababu ninawahangaikia ninyi.

21 Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, Je, hamsikii Sheria? **22** Kwa mfano, imeandikwa kwamba Abrahamu alikuwa na wana wawili, mmoja kupitia kijakazi^a na mwingine kupitia mwanamke aliye huru;^b **23** lakini yule wa kijakazi kwa kweli alizaliwa kupitia njia ya asili*^c na yule mwingine wa mwanamke aliye huru kupitia ahadi.^d **24** Mambo haya yanaweza kumaanisha tukio la mfano; kwa maana wanawake hawa wanamaanisha maagano mawili, moja kutoka Mlima Sinai,^e ambalo huzaa watoto kwa ajili ya utumwa na ambalo ni Hagari. **25** Basi Hagari anaamaanisha Sinai,^f mlima ulio Arabia, naye analingana na Yerusalemu la leo, kwa maana liko katika utumwa pamoja na watoto wake. **26** Lakini Yerusalemu la juu liko huru, nalo ni mama yetu.

27 Kwa maana imeandikwa: "Furahi, wewe mwanamke tasa usiyezaa; piga vigelegele vya shangwe, wewe mwanamke usiye na uchungu wa kuzaa; kwa maana watoto wa mwanamke aliye ukiwa ni wengi kuliko wa yule aliye na mume."^g **28** Basi, akina ndugu, ninyi ni watoto wa ahadi kama Isaka alivyokuwa.^h **29** Lakini kama ilivyokuwa wakati huo, yule aliyezaliwa kupitia njia ya asili* alianza kumtesa yule aliyezaliwa kupitia roho,ⁱ ndivyo ilivyo pia sasa.^j **30** Hata hivyo, andiko linasema nini? "Mfukuze kijakazi na mwanawe, kwa maana mwana wa kijakazi hatakuwa

4:23, 29 *Tnn., "kulingana na mwili."

mrithi kamwe pamoja na mwana wa mwanamke aliye huru.”^a **31** Basi, akina ndugu, sisi si watoto wa kijakazi, bali wa yule mwanamke aliye huru.

5 Kristo alituweka huru ili tuwe na uhuru kama huo. Kwa hiyo, simameni imara,^b na msijiache mfungwe tena katika nira ya utumwa.^c

2 Oneni! Mimi, Paulo, nina-waambia kwamba mkitahiri-wa, Kristo hatakuwa na faida kwenu.^d **3** Tena ninatoa ushahidi kwa kila mtu anayetahiriwa kwamba yuko chini ya wajibu wa kuitimiza Sheria yote.^e **4** Mmetenganishwa na Kristo, ninyi mnaojaribu kutangazwa kuwa waadilifu kupitia sheria,^f mmeanguka kutoka kwenye fadhili zake zisizostahiliwa. **5** Kwa upande wetu, kupitia kwa roho tunasubiri kwa hamu uadilifu uliotumainiwa unaotokana na imani. **6** Kwa maana katika muungano na Kristo Yesu, kutahiriwa au kutotahiriwa hakuna faida yoyote,^g bali imani inayotenda kupitia upendo ina faida.

7 Mliukuwa mnakimbia vema,^h Ni nani aliyewazuia kuendelea kuitii kweli? **8** Ushawishi wa namna hii hautoki kwa Yule anayewaita ninyi. **9** Chachu kidogo huchachisha donge zima.ⁱ **10** Nina uhakika kwamba ninyi mlio katika muungano na Bwana/hamtakuja kufikiria jambo tofauti; lakini yule anayewasababishia taabu,^k hata iwe ni nani, atapokea hukumu anayostahili. **11** Na mimi, akina ndugu, ikiwa bado ninahubiri kuhusu kutahiriwa, kwa nini bado ninateswa? Ikiwa ndi-

SURA YA 4

a Mwa 21:10

SURA YA 5

b 1Ko 16:13

Flp 4:1

c Mdo 15:10

d Gal 6:12

e Ro 2:25

Gal 3:10

f Ro 3:20

g 1Ko 7:19

Gal 6:15

Kol 3:10, 11

h 1Ko 9:24

Gal 3:3

i 1Ko 5:6

1Ko 15:33

2Ti 2:16-18

j Yoh 17:20, 21

k Gal 1:7

Safu ya 2

a 1Ko 1:23

b 1Pe 2:16

c 1Ko 9:19

d Law 19:18

Mt 7:12

Mt 22:39

Ro 13:8, 9

Yak 2:8

e Yak 3:14

f Yak 4:1, 2

g Ro 8:5, 13

h Ro 6:12

1Pe 2:11

i Ro 7:15, 19

Ro 7:23

j 1Ko 5:9

Efe 5:3

Kol 3:5

Ufu 2:20

k Mk 7:21, 22

Efe 4:19

2Pe 2:2

Yud 4

l Law 19:26, 31

Kum 18:10, 11

m Kum 21:20, 21

Isa 5:11

vyo, kikwazo cha mti wa mateso^{*a} kimeondolewa. **12** Ningependa watu wanaojaribu kuwaangusha ninyi wajihasi wenyewe.*

13 Akina ndugu, mliitwa kwenye uhuru; lakini msiutumie uhuru huo kama nafasi ya kufuatilia tamaa za mwili,^b bali mtumikiane kupitia upendo.^c **14** Kwa maana Sheria nzima imetimizwa* katika amri hii moja: “Lazima upende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.”^d **15** Lakini, ikiwa mnaendelea kuumana na kuraruana,^e jihadharini ili msije mkaangamizana.^f

16 Lakini ninasema, Endeeleni kutemba kwa roho^g nanyi hamtatenda kwa tamaa za mwili hata kidogo.^h

17 Kwa maana mwili katika tamaa yake unapingana na roho, na roho inapingana na mwili; vitu hivyo vinapingana, hivi kwamba hamfanyi mambo mnayotaka kufanya.ⁱ

18 Isitoshe, ikiwa mnaongozwa na roho, ninyi hamko chini ya sheria.

19 Sasa matendo ya mwili huonekana wazi, nayo ni uasherati,^{*j} uchafu, mwenendo mpotovu,^{*k} **20** ibada ya sanamu, kuwasiliana na roho,^{*l} chuki, mizozo, wivu, milipuko ya hasira, migogoro, migawanyiko, madhehebu, **21** husuda, ulevi,^m karamu zenye vu-

5:11 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:12 *Au “wawe matowashi,” na hivyo wasistahili kufuata sheria ambayo walikuwa wakiitetea. 5:14 *Au labda, “imejumlishwa.” 5:19 *Neno la Kigiriki *pornei*’a. Angalia Kamusi, uku. 2012. *Au “ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu.” Kigiriki, *a-sef’gei*’a. Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:20 *Au “uchawi.”

ругу,* na mambo kama hayo.^a Ninawaonya mapema kuhusu mambo hayo, kama vile nilivyowaonya tayari, kwa mba wale wanaozoea kufanya mambo hayo hawataurithi Ufalme wa Mungu.^b

22 Kwa upande mwingine, tunda la roho* ni upendo, shangwe, amani, subira,[#] fadhili, wema,^c imani, **23** upole, kujizuia.*^d Hakuna sheria dhidi ya mambo kama hayo. **24** Isitoshe, wale walio wa Kristo Yesu wametundika mtni mwili pamoja na mawazo na tamaa zake mbaya.^e

25 Ikiwa tunaishi kwa roho, na tuendele pia kutembea kwa utaratibu kwa roho.^f **26** Tusiwe tukijisifu,^g tusichochee mashindano kati yetu,^h wala tusioneane wivu.

6 Akina ndugu, hata mtu akichukua hatua isiyofaa kabla hajajua, ninyi mlio na sifa za kustahili kiroho jaribuni kumrekebisha upya mtu huyo kwa roho ya upole.ⁱ Lakini kila mmoja wenu aendele kujiangalia,^j kwa kuwa ninyi pia mnaweza kujaribiwa.^k **2** Endeeleni kubebeana mizigo mizito,^l na hivyo mtaitimiza sheria ya Kristo.^m **3** Kwa maana mtu akifikiri yeye ni kitu wakati yeye si kitu,ⁿ anajidanganya mwenyewe. **4** Lakini kila mmoja na achunguze matendo yake mwenyewe,^o kisha atakuwa na sababu ya kushangilia kuhusiana na yeye mwenyewe, na si kwa kujilinganisha na mtu mwingine.^p **5** Kwa maana kila mtu

5:21 *Au "karamu za kupindukia." 5:22 *Au "sifa zinazotokezwa na roho." #Au "ustahimilivu." 5:23 *Au "kujidhibiti; kujizuia."

SURA YA 5

a 1Pe 4:3

b 1Ko 6:9,10

c Efe 5:9

d Yak 3:17

e Ro 6:6

f Ro 8:4

g Flp 2:3

h Mhu 4:4

1Ko 4:7

Gal 6:4

SURA YA 6

i Met 15:1

Kol 3:12

1Ti 6:11

Tit 3:2

j 1Ko 10:12

k Yak 3:2

l 1Th 5:14

m Yoh 13:34

Yoh 15:12

1Yo 4:21

n Ro 12:3

o 2Ko 13:5

p Gal 5:26

Safu ya 2

a Ro 14:4

2Ko 5:10

b Mt 10:9,10

Lu 10:7

Ro 15:27

1Ko 9:11,14

c Ro 2:6-8

d Ro 8:6,13

e Ebr 3:14

Ebr 12:3

Ufu 2:10

f Yak 2:10

ataubeba mzigo* wake mwenyewe.^a

6 Zaidi ya hayo, mtu yeyote anayefundishwa* neno na ashiriki katika mambo yote mema pamoja na yule anayetoa fundisho hilo.^{#b}

7 Msipotoshwe: Mungu si wa kudhahikiwa. Kwa maana lolote analopanda mtu, ndilo atakalovuna pia;^c **8** kwa sababu yule anayepanda kwa mwili wake atavuna uharibifu kutokana na mwili wake, lakini yule anayepanda kwa roho, atavuna uzima wa milele kutokana na roho.^d **9** Basi tusife moyo katika kufanya mema, kwa maana kwa wakati unao-faa tutavuna ikiwa hatutachoka kabisa.*^e **10** Basi, tukiwa bado na nafasi,* acheni tuwatendee watu wote mema, na hasa wale ambao ni ndugu zetu katika imani.

11 Oneni kwamba nime-waandikia kwa herufi kubwa kwa mkonu wangu mwenyewe.

12 Wote wanaotaka kujionyesha kuwa wazuri katika mwili* ndio wanaojaribu kuwalazimisha mtahiriwe, waki-fanya hivyo ili tu wasiteswe kwa ajili ya mti wa mateso* wa Kristo. **13** Kwa maana hata wale wanaotahiriwa ha-waishiki Sheria,^f lakini wana-taka mtahiriwe ili wawe na sababu ya kujisifu kuhusu mwili wenu. **14** Lakini sitajisifu kamwe, isipokuwa katika mti

6:5 *Au "mzigo wa wajibu." 6:6 *Au "anayefundishwa kwa mdomo." #Au "fundisho hilo la mdomo." 6:9 *Au "hatutakufa moyo." 6:10 *Tnn., "wakati unao-faa." 6:12 *Au "wanaotaka kuonekana wazuri kwa nje." #Angalia Kamusi, uku. 2012.

wa mateso* wa Bwana wetu Yesu Kristo,^a ambaye kupitia kwake ulimwengu umeuawa[#] kuhusiana nami, nami kuhusiana na ulimwengu. **15** Kwa maana kutahiriwa si kitu wala kutotahiriwa,^b bali kiumbe kipa ndicho kitu.^c **16** Na wale wote wanaotembea kwa uta-

6:14 *Angalia Kamusi, uku. 2012. [#]Au “umeuawa kwenye mti.”

SURA YA 6

a 1Ko 2:2

b 1Ko 7:19
Gal 5:6
Kol 3:10, 11c 2Ko 5:17
Efe 2:10

Safu ya 2

a Ro 9:6

b 2Ko 4:10
Flp 3:10

ratibu kwa kanuni hii ya mwenendo, juu yao na kuwe na amani na rehema, ndiyo, juu ya Israeli wa Mungu.^a

17 Kuanzia sasa mtu yeyote asinitaabishe, kwa maana ninabeba mwilini mwangu alama za mtumwa wa Yesu.^b

18 Akina ndugu, fadhili zisizostahiliwa za Bwana wetu Yesu Kristo ziwe pamoja na roho mnyoonyesha. Amina.

KWA

WAEFESO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1, 2)
Baraka za kiroho (3-7)
Kuvikusanya vitu vyote katika Kristo (8-14)
“Usimamizi” katika nyakati zilizowekwa (10)
Kutiwa muhuri kwa roho kama “rehani ya mapema” (13, 14)
Paulo amshukuru Mungu kwa sababu ya imani ya Waefeso na kusali kwa ajili yao (15-23)
- 2 Wafanywa kuwa hai pamoja na Kristo (1-10)
Ukuta unaotenganisha waharibiwa (11-22)
- 3 Siri takatifu ingetia ndani Watu wa Mataifa (1-13)
Watu wa Mataifa ni warithi wenzii pamoja na Kristo (6)

Kusudi la Mungu la milele (11)
Sala kwa ajili ya Waefeso ili wapate hekima (14-21)

- 4 Umoja katika mwili wa Kristo (1-16)
Zawadi katika wanadamu (8)
Utu wa zamani na utu mpya (17-32)
- 5 Usemi na mwenendo safi (1-5)
Tembeeni kama watoto wa nuru (6-14)
Mjazwe roho (15-20)
Tumieni vizuri kabisa wakati wenu (16)
Ushauri kwa waume na wake (21-33)
- 6 Ushauri kwa watoto na wazazi (1-4)
Ushauri kwa watumwa na mabwana (5-9)
Mavazi kamili ya silaha kutoka kwa Mungu (10-20)
Salamu za mwisho (21-24)

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kupitia mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu walio huko Efeso^a na walio waaminifu katika muungano na Kristo Yesu:

SURA YA 1

a Ufu 2:1, 3

2 Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

3 Asifiwe Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwa

kuwa ametubariki kwa kila baraka ya kiroho katika mahali pa kimbangu katika muungano na Kristo,^a **4** kama alivyotuchagua tuwe katika muungano naye* kabla ya kuweka msingi wa ulimwengu, ili tuwe watakatifu na bila dosari^b mbele zake katika upendo. **5** Kwa maana alituagiza awali^c tufanywe kuwa wanawe mwenyewe^d kupitia Yesu Kristo, kulingana na mapenzi yake mema na kusudi lake,^e **6** kwa sifa ya fadhili zake zisizostahiliwa^f zenye utukufu alizotupatia kwa fadhili kupitia mpendwa wake.^g **7** Kupitia kwake tunaachiliwa huru kwa njia ya fidia kupitia damu ya huyo,^h ndiyo, msamaha wa makosa yetu,ⁱ kulingana na utajiri wa fadhili zake zisizostahiliwa.

8 Alituzidishia fadhili zisizostahiliwa katika hekima yote na uelewaji,* **9** kwa kutujulisha siri takatifu^j ya mapenzi yake. Ni kulingana na mapenzi yake mema aliyokusudia mwenyewe **10** kwa ajili ya usimamizi* kwenye nyakati kamili zilizowekwa, kuku-sanya pamoja vitu vyote katika Kristo, vitu vilivyo mbinguni na vitu vilivyo duniani.^k Ndiyo, katika yeye **11** ambaye tuko katika muungano naye na tulihasabiwa kuwa warithi,^l kwa kuwa tuliagizwa awali kulingana na kusudi la yule anayetimiza mambo yote kama anavyoamua kulingana na mapenzi yake, **12** ili sisi tulio wa kwanza kumtumaini Kristo tutumikie kwa ajili ya sifa ya utukufu wake. **13** Lakini ninyi pia mlimtu-

1:4 *Yaani, pamoja na Kristo. 1:8 *Au "akili nzuri." 1:10 *Au "kusimamia mambo."

SURA YA 1

a Efe 2:6

b Efe 5:25-27

c 2Th 2:13
1Pe 1:2d Ro 8:15, 29
Ro 8:23

e Ro 8:28

f Ro 3:24

g Yoh 3:35

h Mdo 20:28
Ro 3:25
Ufu 5:9i Mdo 13:38
Kol 1:14
Kol 2:13

j Ro 16:25, 26

k Flp 2:9, 10
Kol 1:19, 20l Ro 8:17
Efe 3:5, 6

Safu ya 2

a 2Ko 1:22
Efe 4:30
Ufu 7:4b 2Ko 5:5
1Pe 1:3, 4

c 1Pe 2:9

d Ro 8:23
1Ti 2:5, 6e Kol 1:9
1Ti 2:3, 4

f 1Pe 1:3, 4

g 2Ko 13:4

h Zb 110:1
Mdo 7:55i Mdo 4:12
Flp 2:9-11j Zb 8:6
1Ko 15:27
Ebr 2:8

maini baada ya kulisia neno la kweli, habari njema kuhusu wokovu wenu. Baada ya kuamini, mlitiwa muhuri^a kupitia kwake kwa roho takatifu iliyoahidiwa, **14** ambayo ni rehani ya mapema* ya urithi wetu,^b kwa kusudi la kuachilia huru mali ya Mungu mwenyewe^c kupitia fidia,^d kwa sifa yake yenye utukufu.

15 Hiyo ndiyo sababu mimi pia, kwa kuwa nimesikia kuhusu imani mliyo nayo katika Bwana Yesu na upendo mnaowaonyesha watakatifu wote, **16** siachi kamwe kutoa shukrani kwa ajili yenu. Ninaendelea kuwataja katika sala zangu, **17** ili Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape roho ya hekima na ya ufunuo katika ujuzi sahihi kumhusu.^e **18** Ameyatia nuru macho ya moyo wenu, ili mjue tumaini alilowaitia, utajiri wenye utukufu ambao amewekea watakatifu kuwa urithi,^f **19** na jinsi nguvu zake kutuelekea sisi waamini zilivyo kuu zaidi.^g Ni kulingana na utendaji wa uwezo wa nguvu zake, **20** ambao alitumia kuhusiana na Kristo alipomfufua kutoka kwa wafu na kumketisha kwenye mkono wake wa kuume^h katika mahali pa kimbangu, **21** juu kuliko kila serikali na mamla-ka na nguvu na utawala na kila jina linalotajwa,ⁱ si katika mfumo huu wa mambo* tu, bali pia katika ule unakuja. **22** Alivitiisha pia vitu vyote chini ya miguu yake^j na

1:14 *Au "malipo ya awali; uthibitisho (dhamana) wa kile kitakachokuja." 1:21 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo."

kumfanya kuwa kichwa juu ya vitu vyote kuhusiana na kutaniko,^a **23** ambalo ni mwili wake,^b ujazo wake anayejaza vitu vyote katika vyote.

2 Zaidi ya hayo, Mungu aliwafanya muwe hai, ingawa mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu,^c **2** ambazo wakati fulani mlitembea ndani yake kulingana na mfumo wa mambo* wa ulimwengu huu,^d kulingana na mtawala wa mamlaka ya hewa,^e roho^f ambayo sasa inafanya kazi katika wana wa kutotii. **3** Ndiyo, wakati fulani sisi sote tuliendesha miongoni mwao kupatana na tamaa za mwili wetu,^g tukifanya mapenzi ya mwili na ya fikira zetu,^h nasi kiasili tulikuwa watoto wa ghadhabuⁱ kama wale wengine. **4** Lakini Mungu, akiwa tajiri katika rehema,^j kwa sababu ya upendo wake mwingi aliotupenda nao,^k **5** alitufanya hai pamoja na Kristo, hata tulipokuwa wafu katika makosa^l—mmeokolewa kupitia fadhili zisizostahiliwa. **6** Isitoshе, alituinua pamoja na kutuketisha pamoja mahali pa kimbungu katika muungano na Kristo Yesu,^m **7** ili kwenye mifumo ya mambo* inayokuja aonyeshe utajiri mwingi zaidi wa fadhili zake zisizostahiliwa katika neema yakeⁿ kutuelekea katika muungano na Kristo Yesu.

8 Kwa fadhili hizi zisizostahiliwa, ninyi mmeokolewa kupitia imani,ⁿ na si ninyi mliofanya hivyo; badala yake, ni zawadi ya Mungu. **9** Hapana, si kutokana na matendo,^o

2:2 *Au "mwenendo." 2:7 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo." *Au "kibali chake."

SURA YA 1

a Mt 28:18
Efe 5:23
Kol 1:18

b Ro 12:5
Efe 4:16

SURA YA 2

c Kol 2:13

d Ro 12:2
Efe 4:17

e Yoh 12:31

f 1Ko 2:12

g 1Ko 6:9-11

h 1Pe 4:3

i Yoh 3:36

j Zb 145:9

k Ro 5:8
1Yo 4:9,19

l Kol 2:12,13

m Efe 1:3

n Ro 4:16

o Ro 3:20

Safu ya 2

a Gal 6:15

b Efe 1:3, 4

c Ro 9:4

d Isa 65:1

e Kol 1:19, 20

f Kol 3:11

g Law 20:26
Kol 2:13, 14

h 1Ko 12:12
Gal 3:28

i Ebr 12:2

j Mdo 10:28

ili mtu yeyote asiwe na saba-bu za kujisifu. **10** Sisi ni kazi ya mikono* ya Mungu na tuliumbwa^a katika muungano na Kristo Yesu^b kwa ajili ya matendo mema, ambayo Mungu aliamua awali ili tutembee katika hayo.

11 Kwa hiyo, kumbukeni kwamba wakati fulani ninyi, watu wa mataifa kwa kuzaliwa, mlikuwa mkiitwa "watu wasiotahiriwa" na wale walioitwa "watu waliotahiriwa," kutahiriwa ambako kumefanywa mwilini kwa mikono ya wanadamu. **12** Wakati huo hamkuwa na Kristo, mlikuwa mmetengwa na taifa la Israeli, mlikuwa wage-ni kwa maagano ya ahadi;^c hamkuwa na tumaini na mlikuwa bila Mungu katika ulimwengu.^d **13** Lakini sasa katika muungano na Kristo Yesu ninyi ambao wakati fulani mlikuwa mbali sana, mmekuwa karibu kupitia damu ya Kristo. **14** Kwa maana yeye ni amani yetu,^e yule aliyefanya vile vikundi viwili kuwa kimoja^f na kuuharibu ukuta wa katikati uliowatenganisha.^g **15** Kupitia mwili wake aliu-futa uadui, ile Sheria iliyokuwa na amri na maagizo, ili afanye vile vikundi viwili katika muungano na yeye mwenyewe viwe mtu mmoja mpya^h na kufanya amani, **16** na kuvipatanisha kikamili vile vikundi viwili vya watu katika mwili mmoja kwa Mungu kupitia mti wa mateso,^{*i} kwa sababu alikuwa amea ule uaduiⁱ kupitia yeye mwenyewe. **17** Naye alikuja na kuwata-ngazia habari njema ya ama-

2:10 *Au "matokeo ya kazi." 2:16 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

ni ninyi mliokuwa mbali sana, na amani kwa wale waliokuwa karibu, **18** kwa sababu kupitia kwake, sisi, vikundi viwili vya watu, tuna uhuru wa kumkaribia Baba kwa roho moja.

19 Basi ninyi si wageni tena na watu wa mataifa ya kigeni,^a bali ninyi ni raia wenzi^b wa watakatifu na ni washiriki wa nyumba ya Mungu,^c **20** nanyi mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii,^d naye Kristo Yesu mwenyewe ndiye jiwe la msingi la pembeni.^e **21** Katika muungano naye, jengo lote likiwa limeunganishwa kwa upatano,^f linakua ili kuwa hekalu takatifu kwa ajili ya Yehova.*^g **22** Katika muungano naye, ninyi pia mnajengwa pamoja muwe mahali pa Mungu pa kukaa kupitia roho.^h

3 Kwa sababu hii, mimi Paulo, mfungwaⁱ wa Kristo Yesu kwa ajili yenu, watu wa mataifa— **2** ikiwa, kwa kweli, mmesikia kuhusu usimamiziⁱ wa fadhili zisizostahiliwa za Mungu ambao nilipewa kwa ajili yenu, **3** kwamba nilijulishwa siri takatifu kupitia ufunuo, kama vile nilivyoandika kwa ufupi hapo mwanzoni. **4** Basi mnaposoma jambo hili, mnaweza kuona jinsi ninavyoelewa siri takatifu^k ya Kristo. **5** Katika vizazi vingine wanadamu hawakujulishwa siri hii kama vile ambavyo sasa imefunuliwa kwa mitume wake watakatifu na manabii kupitia roho,^l **6** yaani, kwamba watu wa mataifa, katika muungano na Kristo Yesu na kupitia habari njema, wawe warithi na viungo vya mwili

2:21 * Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 2

a Efe 2:12

b Flp 3:20

c 1Ti 3:15
Ebr 3:6

d 1Ko 12:28

e Isa 28:16

f Kol 2:19

g 1Ko 3:16
1Ko 6:19

h 1Pe 2:5

SURA YA 3

i Efe 4:1

j 1Ko 9:16,17
Kol 1:25,26k 1Ko 4:1
Efe 6:19l Ro 11:25
Ro 16:25,26

Safu ya 2

a Efe 2:15,16

b Kol 1:25-27

c 1Ko 15:9

d 1Ti 1:13,14

e Efe 1:9,10

f 1Pe 1:10,12

g 1Pe 2:9

h Efe 1:11

i Yoh 14:6
Ebr 4:15,16

j 2Ti 2:10

k 2Ko 4:16

l Yoh 14:23

uleule^a na washiriki wa ahadi pamoja nasi. **7** Mimi nilikuja kuwa mhudumu wa hilo kulingana na zawadi ya bure ya Mungu ya fadhili zisizostahiliwa nilizopewa kupitia utendaji wa nguvu zake.^b

8 Mimi, niliye mdogo kuliko aliye mdogo zaidi kati ya watakatifu wote,^c nilipewa fadhili hizi zisizostahiliwa,^d ili niwatangazie mataifa habari njema kuhusu utajiri usiopimika wa Kristo **9** na kufanya kila mtu aone usimamizi wa siri takatifu^e ambayo imefichwa kwa vizazi na vizazi katika Mungu, aliyumba vitu vyote. **10** Ilikuwa hivyo ili sasa, kupitia kutaniko,^f serikali na mamlaka zilizo mahali pa kimbingu zijulishwe hekima ya Mungu inayoonekana kwa njia nyingi sana.^g **11** Hii ni kulingana na kuseudi la milele alilofanyiza kuhusiana na Kristo,^h Yesu Bwana wetu, **12** ambaye kupitia kwake tuna uhuru huu wa kusema na uhuru wa kukaribiaⁱ tukiwa na uhakika kupitia imani yetu kwake. **13** Basi ninawaomba msife moyo kwa sababu ya dhiki zangu kwa ajili yenu, kwa maana zinamaanisha utukufu kwenu.^j

14 Kwa sababu hiyo ninampigia Baba magoti, **15** ambaye kila familia mbinguni na duniani hupata jina kutoka kwake. **16** Ninasali kwamba awezeshe kulingana na wingi wa utukufu wake ili mfanywe kuwa na uwezo katika mtu mliye kwa ndani,^k mkiwa na nguvu kupitia roho yake, **17** na kupitia imani yenu muwe na Kristo akikaa katika mioyo yenu kwa upendo.^l Iweni na

mizizi^a na kuimarishwa juu ya ule msingi,^b **18** ili pamoja na watakatifu wote mweze kufahamu kikamili upana na urefu na kimo na kina, **19** na kuujuua upendo wa Kristo,^c unaozidi ujuzi, ili mjawe na ujazote wote ambao Mungu hutoa.

20 Basi kwa yule anayeweza, kulingana na nguvu zake zinazotenda ndani yetu,^d kufanya kwa wingi zaidi kupita mambo yote tunayoomba au tunayofikiri,^e **21** na awe na utukufu kupitia kutaniko na kupitia Kristo Yesu kwa vizazi vyote milele na milele. Amina.

4 Kwa hiyo, mimi mfungwa^f katika Bwana, ninawasihi mtembee kwa kustahili^g mwito mliopokea, **2** kwa unyenyekevu^{*h} wote na upole, kwa subira,ⁱ mkivumiliana kwa upendo,^j **3** mkijitahidi sana kudumisha roho ya umoja katika kifungo cha muungano cha amani.^k **4** Kuna mwili mmoja,^l na roho moja,^m kama mliyoyitwa kwenye tumaini moja;ⁿ **5** Bwana mmoja,^o imani moja, ubatizo mmoja; **6** Mungu mmoja ambaye ni Baba wa wote, aliye juu ya wote, na kupitia wote na katika wote.

7 Basi kila mmoja wetu alionyeshwa fadhili zisizostahiliwa kulingana na jinsi Kristo alivyopima zawadi hiyo ya bure.^p **8** Kwa maana inasema: "Alipopanda juu alichukua mateka; alitoa wanaume kuwa zawadi."^q **9** Basi neno "alipopanda," linamaanisha nini? Linamaanisha kwamba pia alishuka chini, yaani, duniani. **10** Yule aliyeshuka ndiye pia aliyepanda^r juu zai-

4:2 *Au "unyenyekevu wa akili."

SURA YA 3

a Kol 2:6, 7

b Kol 1:23

c Ro 8:35

d Kol 1:29

e Mk 11:24

SURA YA 4

f Flm 9

g Flp 1:27

h Mt 11:29

Ro 12:3

Flp 2:3

1Pe 5:5

i 1Th 5:14

j 1Ko 13:4

k 1Ko 1:10

Kol 3:15

l Ro 12:5

m 1Ko 12:4

n 1Pe 1:3, 4

o 1Ko 8:6

1Ko 12:5, 6

p 1Ko 12:11

q Zb 68:18

1Ko 12:28

Efe 4:11

r Mdo 1:9

1Ti 3:16

Safu ya 2

a Ebr 9:24

b Mt 10:2-4

c 1Ko 12:28

d Mdo 21:8

e Mdo 13:1

Yak 3:1

f 1Ko 14:26

g 1Ko 14:20

h Ebr 13:9

i 1Ko 11:3

Kol 1:18

j 1Ko 12:27

k Kol 2:19

l 1Pe 4:3

m Ro 1:21

di ya mbingu zote,^a ili atimize mambo yote.

11 Naye alitoa wengine wawe mitume,^b wengine manabii,^c wengine waeneza injili,^{*d} wengine wachungaji na walimu,^e **12** ili kuwarekebishisha^{*} watakatifu, kwa ajili ya kutimiza huduma, na kuujuua mwili wa Kristo,^f **13** mpaka sote tuwe na umoja^{*} katika imani na tuwe na ujuzi sahihi kumhusu Mwana wa Mungu, na kuwa mtu aliyekomaa kabisa,^g na kufikia kiwango cha kimo kamili cha Kristo. **14** Basi tusiwe tena watoto, tukirushwa huku na huku kama kwa mawimbi na kupeperushwa na kila upepo wa fundisho^h kwa udanganyifu wa watu, kupitia ujanja na njia za hila. **15** Lakini tukisema ukweli, kupitia upepo na tuendeleo kukua katika mambo yote ndani ya Kristo, ambaye ni kichwa,ⁱ **16** Kupitia kwake mwili wote/ unaunganishwa na kushirikiana kila kiungo kinapofanya kazi yake. Na kila kiungo kinapofanya kazi vizuri, hilo linafanya mwili ukue na kujijenga katika upendo.^k

17 Basi ninasema na kushuhudia katika Bwana, kwamba msiishi tena kama watu wa mataifa wanavyoishi,^l katika ubatili wa akili zao.^m **18** Wako gizani kiakili na wametenganishwa na uzima ambao ni wa Mungu, kwa sababu ya ujinga ulio ndani yao na kwa sababu ya ugumu wa^{*} mioyo yao. **19** Kwa kuwa wamepotoka kabisa kimaadi-

4:11 *Au "wahubiri wa habari njema."
4:12 *Au "kuwazoeza." 4:13 *Au "muungano." 4:18 *Tnn., "kukosa hisia katika."

li, wamejiingiza katika mwendo mpotovu*^a na kufanya mambo machafu ya kila namna kwa pupa.

20 Lakini ninyi hamkujifunza kwamba Kristo yuko hivyo, **21** ikiwa kwa kweli mli-msikia na kufundishwa kupitia kwake, kama vile kweli ilivyo katika Yesu. **22** Mlifundishwa kuvua utu wa zamani^b unaopatana na mwendo wenu wa zamani na ambao unaharibiwa na tamaa zake za udanganyifu.^c **23** Na mnapaswa kuendelea kufanywa upya katika nguvu zinazoongoza akili zenu,^{*d} **24** na mnapaswa kuvaa utu mpya^e uliombwa kupatana na mapenzi ya Mungu katika uadilifu wa kweli na ushikamamifu.

25 Kwa hiyo, kwa sababu mmeacha udanganyifu, semeni ukweli kila mmoja na mwenzake,^f kwa sababu sisi ni viungo vya mwili mmoja.^g **26** Iweni na hasira, lakini msitende dhambi;^h jua lisitue mkiwa bado mkekasi-rika;ⁱ **27** msimpe Ibilisi nafasi.^j **28** Mwizi asiibe tena; badala yake afanye kazi kwa bidii, akifanya kazi njema kwa mikono yake,^k ili awe na kitu cha kumgawia mtu mwenye uhitaji.^l **29** Neno lililooza lisitoke kinywani mwenu,^m bali neno jema kwa ajili ya kujenga kulingana na uhitaji, ili liwanufaishe wale wanaolisikia.ⁿ **30** Pia, msiwe mkiihuzunisha roho takatifu ya Mungu,^o ambayo kupitia hiyo mmeti-

4:19 *Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki, *a-sef'gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 4:23 *Au "nguvu zinazotawala akili zenu." Tnn., "roho ya akili yenu."

SURA YA 4

a Gal 5:19

b Ro 6:6
Kol 3:9

c Ro 7:23

d Zb 51:10
Ro 12:2

e Kol 3:10

f Zek 8:16
Kol 3:8, 9
Ufu 21:8

g Ro 12:5

h Zb 4:4

i Law 19:17
Kol 3:13

j Yak 4:7

k 2Th 3:10

l Mdo 20:35
1Th 4:11, 12m Mt 15:11
Yak 3:10

n Kol 4:6

o Isa 63:10

Safu ya 2

a Efe 1:13

b Ro 8:23

c Yak 3:14

d Kol 3:8

e Tit 3:2

f Kol 3:12
1Pe 3:8g Mt 6:14
Mt 18:35
Mk 11:25

SURA YA 5

h Mt 5:48

Lu 6:36

i 1Ko 16:14

j Yoh 13:34
1Yo 3:23

k Kut 29:18

l 1Ko 5:11
Kol 3:5

m 1Th 4:3

n Kol 3:8

o 1Th 5:18

p Mdo 15:28, 29

q 1Ti 3:8
Tit 1:7r 1Ko 6:9, 10
Gal 5:19, 21

wa muhuri^a kwa ajili ya siku ambayo mtawekwa huru kupitia fidia.^b

31 Acheni kabisa kila aina ya chuki yenye uhasama,^c hasira, ghadhabu, kufoka, matusi,^d na mambo yote yanayodhuru.^e **32** Bali mtendane kwa fadhili, huruma nyoro-ro,^f mkisameheana kwa hiari kama vile Mungu aliyowasamehe ninyi kwa hiari kupitia Kristo.^g

5 Kwa hiyo, iweni waigaji wa Mungu,^h kama wato-to wapendwa, **2** na mwendelelee kutembea katika upendo,ⁱ kama vile Kristo pia aliyotupenda sisi*^j na kujitoa mwenyewe kwa ajili yetu^k kuwa toleo na dhahibu yenye harufu tamu kwa Mungu.^k

3 Uasherati* na kila namna ya ukosefu wa usafi au pupa visitajwe kamwe miongoni mwenu,^l kama inavyowafaa watu watakatifu,^m **4** wala mwenendo wa aibu wala maneno ya kipumbavu wala mizaha michafuⁿ—mambo yasiyofaa—badala yake, kutoa shukrani.^o **5** Kwa maana mnajua hili, nanyi mnalitambua wenyewe, kwamba hakuna mwasherati*^p au mtu asiye safi au mtu mwenye pupa,^q maana yake mtu anayeabudu sanamu, aliye na urithi wowote katika Ufalme wa Kristo na wa Mungu.^r

6 Mtu yeyote asiwadanganye kwa maneno matupu, kwa maana ghadhabu ya Mungu inakuja juu ya wana wa kutotii kwa sababu ya mambo hayo. **7** Kwa hiyo, msishirikiane

5:2 *Au labda, "ninyi." #Au labda, "yenu." 5:3 *Neno la Kigiriki *pornei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:5 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Uasherati."

nao; **8** kwa kuwa wakati fulani mlikuwa giza, lakini sasa ninyi ni nuru^a kuhusiana na Bwana.^b Endeleeni kute-mbea kama watoto wa nuru, **9** kwa maana tunda la nuru lina kila namna ya wema na uadilifu na kweli.^c **10** Endeleeni kuhakikisha jambo linalokubalika^d kwa Bwana; **11** na mwache kushiriki katika matendo yasiyozaa matunda, ambayo ni ya giza;^e badala yake, myafunue jinsi yalivyo. **12** Kwa maana mambo wanayotenda katika siri ni aibu hata kuyataja. **13** Basi mambo yote yanayofunuliwa yanawekwa wazi* na nuru, kwa maana kila jambo linalowekwa wazi ni nuru. **14** Kwa hiyo, inasemwa: "Amka, wewe unayelala usingizi, na ufufuke kutoka kwa wafu,^f na Kristo atakuangazia."^g

15 Basi endeleeni kuangalia sana jinsi mnavyotembea, si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima, **16** mkiutumia vizuri kabisa wakati wenu,^{*h} kwa sababu siku hizi ni zenye uovu. **17** Kwa hiyo acheni kuwa watu wasio na akili, bali endeleeni kuyafahamu mapenzi ya Yehova.^{*i} **18** Pia, msilewe divai,^j ambayo ina upotovu,^{*k} bali endeleeni kujazwa roho. **19** Mkizungumza kati yenu[#] kwa zaburi, sifa kwa Mungu, na nyimbo za kiroho, mkiiimba^k na kupiga muziki^l katika mioyo yenu kwa Yehova,^{*m} **20** sikuzote mkimtolea shukraniⁿ Mungu na Baba yetu

5:13 *Au "yanakaripiwa." 5:16 *Tnn., "mkijinunulia wakati uliowekwa." 5:17, 19 *Angalia Nyongeza A5. 5:18 *Au "haina adabu." 5:19 #Au labda, "mkizungumzia."

SURA YA 5

- a Mt 5:16
Yoh 12:36
- b 1Pe 2:9
- c Gal 5:22, 23
- d Ro 12:2
- e Ro 13:12, 13
2Ko 6:14
- f Efe 2:1
Kol 2:13
- g Yoh 8:12
- h Kol 4:5
- i Ro 12:2
1Th 4:3
1Pe 4:2
- j Isa 5:11
- k Yak 5:13
- l Zb 33:2, 3
- m Mdo 16:25
Kol 3:16
- n 1Th 5:18

Safu ya 2

- a Kol 3:17
- b Flp 2:3
1Pe 5:5
- c Kol 3:18
Tit 2:4, 5
1Pe 3:1
- d Ro 7:2
- e 1Ko 11:3
- f 1Pe 3:7
- g Mdo 20:28
- h Yoh 17:17
- i Tit 2:13, 14
- j Efe 1:4
Kol 1:21, 22
- k Ro 12:5
Efe 1:22, 23
- l Mwa 2:24
Mt 19:5
- m Efe 1:9, 10
Kol 1:26, 27
- n Efe 3:5, 6

kwa ajili ya mambo yote katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo.^a

21 Jitiisheni kila mmoja kwa mwenzake^b katika kumwogopa Kristo. **22** Wake na wajitiishe kwa waume zao^c kama kwa Bwana, **23** kwa sababu mume ni kichwa cha mke wake^d kama vile Kristo alivyo kichwa cha kutaniko,^e yeye akiwa mwokozi wa mwili huu. **24** Kwa kweli, kama vile kutaniko linavyojitiisha kwa Kristo, wanawake pia wanapaswa kujitiisha kwa waume zao katika mambo yote. **25** Enyi waume, endeleeni kuwapenda wake zenu,^f kama vile Kristo pia alivyolipenda kutaniko na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake,^g **26** ili alitakase, akilisafisha na kulio-sha kwa maji kupitia neno,^h **27** ili kujipa mwenyewe kutaniko likiwa na fahari, bila doa au kunyanzi au lolote kati ya mambo hayo,ⁱ bali likiwa takatifu na bila dosari.^j

28 Vivyo hivyo, waume wanapaswa kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Mwanamume anayempenda mke wake anajipenda mwenyewe, **29** kwa maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake, bali huulisha na kuutunza, kama vile Kristo anavyolitendea kutaniko, **30** kwa kuwa sisi ni viungo vya mwili wake.^k **31** "Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye atashikamana* na mke wake, na hao wawili watakuwa mwili mmoja."^l **32** Siri hii takatifu^m ni kubwa. Sasa ninazungumza kuhusu Kristo na kutaniko.ⁿ **33** Hata hi-

5:31 *Au "atabaki."

vyo, kila mtu kati yenu anapaswa kumpenda mke wake^a kama anavyojipenda mwenyewe; kwa upande mwingine, mke anapaswa kumheshimu sana mume wake.^b

6 Enyi watoto, watiini wazazi wenu^c katika muungano na Bwana, kwa maana hilo ni jambo la uadilifu. **2** “Mheshimu baba yako na mama yako,”^d hiyo ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi: **3** “Ili mambo yakuende vema* nawe ukae muda mrefu duniani.” **4** Nanyi akina baba, msiwe mkiwakasirisha watoto wenu,^e bali endeleeni kuwalea katika nidhamu^f na maagizo ya* Yehova.^g

5 Enyi watumwa, watiini mabwana wenu wanadamu,^{*h} kwa kuogopa na kutetemeka kwa unyoofu wa miyo yenu, kama vile kwa Kristo, **6** si wakati tu mnapotazamwa, ili tu kuwapendeza wanadamu,^{*i} bali kama watumwa wa Kristo mkifanya mapenzi ya Mungu kwa nafsi[#] yote.^j **7** Tumikieni mkiwa na mtazamo mzuri, kama kwa Yehova,^{**k} na si kwa wanadamu, **8** kwa maana mnajua kwamba wema wote ambao kila mtu hufanya, Yehova[#] atamlipa wema huo,^l iwe ni mtumwa au mtu huru. **9** Pia, enyi mabwana, endeleeni kuwatendea kwa njia hiyohiyo, bila kuwatisha, kwa maana mnajua kwamba Bwana wao na wenu pia yuko mbinguni,^m naye hana ubaguzi wowote.

6:3 *Au “Ili ufanikiwe.” **6:4** *Au “mwellekezo wa; mwongozo wa.” Tnn., “kuweka katika akili.” **6:4, 7, 8** #Angalia Nyongeza A5. **6:5** *Tnn., “wa kimwili.” **6:6** *Tnn., “si kwa njia ya utumishi wa macho ili kuwapendeza wanadamu.” #Angalia Kamusi, uku. 2012, “Nafsi.”

SURA YA 5

a Kol 3:19

b 1Pe 3:5, 6

SURA YA 6

c Met 1:8

Met 6:20

Kol 3:20

d Kut 20:12

Kum 5:16

Met 20:20

Met 23:22

Mt 15:4

e Kol 3:21

f Met 13:24

g Kum 6:6, 7

Met 3:11

Met 19:18

Met 22:6

h 1Ti 6:1

1Pe 2:18

i Kol 3:22

j Lu 10:27

k 1Ko 10:31

l Kol 3:23, 24

m 1Ko 7:22

Safu ya 2

a Efe 3:16

b Ro 13:12

c 2Ti 4:7

d 2Pe 2:4

e 2Ko 6:4, 7

f Isa 11:5

g Met 4:23

Isa 59:17

h Isa 52:7

Ro 10:15

i 1Yo 5:4

j 1Pe 5:8, 9

k Isa 59:17

1Th 5:8

l Ebr 4:12

m Kol 4:2

n Yud 20

10 Mwishowe, endeleeni kujipatia nguvu^a katika Bwana na katika uwezo wa nguvu zake. **11** Vaeni mavazi kamili ya silaha^b kutoka kwa Mungu ili mweze kusimama imara dhidi ya matendo yenye hila ya* Ibilisi; **12** kwa sababu tunapambana,^{*c} si dhidi ya damu na mwili, bali dhidi ya serikali, dhidi ya mamlaka, dhidi ya watawala wa ulimwengu wa giza hili, dhidi ya majeshi ya roho waovu^d katika mahali pa kimbangu. **13** Kwa sababu hiyo chukueni mavazi kamili ya silaha kutoka kwa Mungu,^e ili mweze kupinga katika ile siku ya uovu, na baada ya kutimiza mambo yote, mweze kusimama imara.

14 Kwa hiyo, simameni imara, mkiwa mmejifunga kiunoni mshipi wa ile kweli,^f mkiwa mmevaa bamba la kifuani la uadilifu,^g **15** na mkiwa mmevaa viatu miguuni tayari kutangaza habari njema ya amani.^h **16** Mbali na mambo hayo, chukueni ngao kubwa ya imani,ⁱ ambayo kwa kuitumia mtaizima mishale yote inayowaka moto* ya yule mwovu.^j **17** Pia, pokeeni kofia ya chuma ya wokovu,^k na upanga wa roho, yaani, neno la Mungu,^l **18** na kwa kila namna ya sala^m na dua mkiendelea kusali kila wakati katika roho.ⁿ Na hivyo kaeni macho, daima mkiomba dua kwa ajili ya watakatifu wote. **19** Pia, msali kwa ajili yangu, kwamba ninapofungua kinywa changu nipewe maneno, ili niweze

6:11 *Au “njama za.” **6:12** *Tnn., “tunapigana mweleka.” **6:16** *Au “makombora.”

kuzungumza kwa ujasiri nina-
pojulisha siri takatifu ya ha-
bari njema,^a **20** ambayo kwa
ajili yake ninatenda kama ba-
lozi^b aliyefungwa minyoro-
ro, na kwamba niweze kuzu-
ngumza kuihusu kwa ujasiri,
kama ninavyopaswa kuzu-
ngumza.

21 Basi ili ninyi pia mjue
kunihusu na jinsi ninavyo-
endelea, Tikiko,^c ndugu mpe-
ndwa na mhudumu mwamini-

SURA YA 6

a Kol 4:3

b 2Ko 5:20

c 2Ti 4:12
Tit 3:12

Safu ya 2

a Kol 4:7,8

fu katika Bwana, atawajulisha
mambo yote.^a **22** Ninamtu-
ma kwenu kwa kusudi hili, ili
mjue jinsi tunavyoendelea na
aifariji mioyo yenu.

23 Akina ndugu na wawe na
amani na upendo pamoja na
imani kutoka kwa Mungu Baba
na Bwana Yesu Kristo. **24** Fa-
dhili zisizostahiliwa na ziwe
pamoja na wote wanaompe-
nda Bwana wetu Yesu Kristo
katika hali ya kutoharibika.

KWA

WAFILIFI

YALIYOMO

- | | |
|--|---|
| <p>1 Salamu (1, 2)
Shukrani kwa Mungu; Sala ya
Paulo (3-11)
Habari njema yasonga mbele licha ya
matatizo (12-20)
Kuishi ni Kristo, kifo ni faida (21-26)
Jiendesheni kwa njia inayostahili habari
njema (27-30)</p> <p>2 Unyenyekevu wa Kikristo (1-4)
Unyenyekevu wa Kristo na kupandishwa
cheo (5-11)
Fanyieni kazi wokovu wenu
wenyewe (12-18)
Kuangaza kama mianga (15)
Kumtuma Timotheo na
Epafrodito (19-30)</p> | <p>3 Uhakika usitegemee mwili (1-11)
Mambo yote ni hasara kwa ajili ya
Kristo (7-9)
Kujinyoosha mbele kuelekea
mradi (12-21)
Uraia mbinguni (20)</p> <p>4 Umoja, kushangilia, mawazo
yanayofaa (1-9)
Msihangaike kuhusu jambo
lolote (6, 7)
Paulo awashukuru Wafilifi kwa
zawadi (10-20)
Salamu za mwisho (21-23)</p> |
|--|---|

1 Paulo na Timotheo, watu-
mwa wa Kristo Yesu, kwa
watakatifu wote katika mu-
ngano na Kristo Yesu walio
huko Filipi,^a pamoja na wa-
ngalizi na watumishi wa hu-
duma.^b

2 Na muwe na fadhili zisi-
zostahiliwa na amani kutoka

SURA YA 1

a Mdo 16:12

b 1Ti 3:1, 8

Safu ya 2

a 1Th 1:2

kwa Mungu Baba yetu na Bwa-
na Yesu Kristo.

3 Sikuzote ninamshukuru
Mungu wangu ninapowaku-
mbuka ninyi **4** katika dua za-
ngu zote kwa ajili yenu nyote.
Ninatoa kila dua kwa
shangwe,^a **5** kwa sababu ya

mchango ambao mmeutoa kwa ajili ya* habari njema tangu siku ya kwanza mpaka sasa. **6** Kwa maana nina uhakika kuhusu jambo hili, kwamba yule aliyeanzisha kazi njema ndani yenu ataikamilisha^a kufikia siku ya Kristo Yesu.^b **7** Ni sawa kwangu kufikiri hivyo kuwahusu ninyi nyote, kwa sababu mko katika moyo wangu, ninyi mlio washirikiki pamoja nami katika fadhili zisizostahiliwa katika vifungo vyangu vya gereza^c na katika kuitetea na kuithibitisha kisheria habari njema.^d

8 Kwa maana Mungu ni shahidi wangu kuhusu jinsi ninavyotamani kuwaona ninyi nyote kwa upendo mwororo kama alio nao Kristo Yesu. **9** Na hili ndilo ninaloendelea kusali, kwamba upendo wenu uwe mwingi zaidi na zaidi^e pamoja na ujuzi sahihi^f na utambuzi kamili;^g **10** kwamba mhakikishe mambo muhimu zaidi,^h ili muwe bila kasoro na msiwe mkiwakwaza wengineⁱ mpaka siku ya Kristo; **11** na kwamba mjazwe tunda la uadilifu, ambalo ni kupitia Yesu Kristo,^j kwa utukufu na sifa kwa Mungu.

12 Basi ninataka mjue, aki-na ndugu, kwamba hali yangu kwa kweli imesaidia kuendeleza habari njema, **13** hivi kwamba vifungo vyangu vya gereza^k kwa ajili ya Kristo vimejulikana wazi^l kati ya Walinzi wote wa Mfalme na watu wengine wote. **14** Sasa aki-na ndugu wengi katika Bwana wamekuwa na uhakika kwa sababu ya vifungo vyangu vya gereza, nao wanaonyesha

1:5 *Au "kwa sababu mmeshiriki kuendeleza."

SURA YA 1

a Flp 2:13

b 1Ko 1:8

c Efe 3:1
Flp 1:13
Kol 4:18
2Ti 1:8
Flm 13d Mdo 24:10, 14
Mdo 25:10-12

e 1Th 3:12

f Yoh 17:3

g Ebr 5:14

h Ro 12:2

i Ro 14:13, 21

j Yoh 15:5

k Efe 3:1

l Mdo 28:30, 31

Safu ya 2

a Flp 1:7

b 2Ko 1:11

c Yoh 15:26

d Ro 14:8
1Pe 4:16

e Gal 2:20

f 1Th 4:14
2Ti 4:8
Ufu 14:13

g 2Ti 4:6

h 2Ko 5:6, 8

uhodari mwingi wa kulisema neno la Mungu bila woga.

15 Ni kweli, wengine wanamhubiri Kristo kwa wivu na kushindana, lakini wengine kwa nia njema. **16** Hao wa mwisho wanamtangaza Kristo kutokana na upendo, kwa maana wanajua kwamba ni-mechaguliwa ili kuitetea habari njema;^a **17** lakini wale wa kwanza hufanya hivyo kutokana na ugomvi, si kwa kusudi safi, kwa maana wanataka kunisababishia dhiki katika vifungo vyangu vya gereza. **18** Matokeo ni nini? Ni kwamba katika kila njia, iwe ni kwa unafiki au ni kwa ukweli, Kristo anatangazwa, nami ninashangilia kuhusu jambo hilo. Kwa kweli, nitaendelea pia kushangilia, **19** kwa maana ninajua hilo litanisaidia kupata wokuvu kupitia dua yenu^b na kwa msaada wa roho ya Yesu Kristo.^c **20** Hilo linapatana na tarajio langu lenye hamu na tumaini kwamba sitaona aibu kwa njia yoyote, bali kwamba kwa uhuru wote wa kusema, sasa Kristo, kama sikuzote hapo mwanzoni, atatukuzwa kupitia mwili wangu, iwe ni kupitia uzima au kupitia kifo.^d

21 Kwa maana kwangu mimi, kuishi ni Kristo^e na kifo ni faida.^f **22** Basi ikiwa nitaendelea kuishi katika mwili, hilo ni tunda la kazi yangu; hata hivyo, mimi sisemi kile nitakachochagua. **23** Ninakabiliwa na mambo haya mawili, kwa maana ninatamani kufunguliwa na kuwa pamoja na Kristo,^g ambako, kwa hakika, ni bora zaidi.^h **24** Hata hivyo, ni muhimu zaidi kwangu kubaki katika mwili

kwa ajili yenu. **25** Basi, nikiwa na uhakika wa jambo hili, ninajua nitabaki na kuendelea pamoja nanyi nyote ili msonge mbele na muwe na shangwe katika imani, **26** ili kwa sababu yangu furaha yenu ifurike katika Kristo Yesu nitakapokuwa tena pamoja nanyi.

27 Ila tu jiendesheni* kwa njia inayostahili habari njema kuhusu Kristo,^a ili kama nitakuja kuwaona au nisipokuja, nisikie kuwahusu na nisikie kwamba mnasimama imara katika roho moja, kwa nafsi moja,^{#b} mkijitahidi pamoja kwa ajili ya imani ya habari njema, **28** bila kuogopeshwa kamwe na wapinzani wenu. Jambo hili ni uthibitisho wa uharibifu^c kwao, lakini wa wokovu kwenu;^d na hili linatoka kwa Mungu. **29** Kwa maana mlipewa pendeleo kwa ajili ya Kristo, si muwe tu na imani katika yeye, bali pia mteseke kwa ajili yake.^e **30** Kwa maana mna pambano kama lile mliloona nikikabili,^f ambalo mnasikia kwamba bado ninakabili.

2 Basi, ikiwa kuna jambo lote la kutia moyo katika Kristo, ikiwa kuna faraja yoyote ya upendo, ikiwa kuna ushirika wowote wa kiroho,* ikiwa kuna upendo mwororo na huruma zozote, **2** fanyeni shangwe yangu ijae kwa kuwa na akili ileile na kuwa na upendo ulleule, mkiwa mmeunganishwa kabisa,* mkiwa na wazo moja akilini.^g **3** Msifanye jambo lolote kwa ugomvi^h au kwa kujisifu,ⁱ bali kwa

1:27 *Au "jiendesheni kama raia." #Au "kwa nia moja." 2:1 *Tnn., "ushirika wowote wa roho." 2:2 *Au "mkiwa mmeunganishwa katika nafsi."

SURA YA 1

a Efe 4:1, 3
Kol 1:10

b Ro 15:5, 6
1Ko 1:10

c 2Th 1:6

d Lu 21:19
2Th 1:4, 5

e Mdo 5:41

f Mdo 16:22, 23
1Th 2:2

SURA YA 2

g 1Ko 1:10
2Ko 13:11
1Pe 3:8

h Flp 1:15, 17
Yak 3:14, 16

i Gal 5:26

Safu ya 2

a Mt 23:11
Efe 4:1, 2
Efe 5:21

b 1Ko 13:4, 5

c 1Ko 10:24
1Ko 10:32, 33

d Mt 11:29
Yoh 13:14, 15

e Kol 1:15
Ebr 1:3

f Yoh 14:28

g Isa 53:2, 3

h Yoh 1:14

i Yoh 10:17
Ebr 2:9
Ebr 5:8

j Gal 3:13

k Isa 52:13
Mdo 2:32, 33

l Mdo 4:12
Efe 1:20, 21

m Yoh 5:22, 23

n Ro 10:9

unyenyeketu* mwaone wengine kuwa bora kuliko ninyi,^a **4** huku mkiangalia, si faida zenu wenyewe,^b bali pia faida za wengine.^c

5 Iweni na mtazamo huu wa akili ambao pia Kristo Yesu alikuwa nao,^d **6** ambaye, ingawa alikuwa katika umbo la Mungu,^e hakufikiria kamwe wazo la kujaribu kuwa sawa na Mungu.^f **7** Hapana, bali alijiondolea hali yake na kuchukua umbo la mtumwa^g na kuwa mwanadamu.^{*h} **8** Zaidi ya hayo, alipokuja akiwa mwanadamu,* alijinyenyekeza na kuwa mtiifu mpaka kifo,ⁱ ndiyo, kifo juu ya mti wa mateso.^{#j} **9** Kwa sababu hiyo, Mungu alimpandisha kwenye cheo cha juu zaidi^k na kumpa kwa fadhili jina lililo juu kuliko kila jina lingine,^l **10** ili katika jina la Yesu kila goti lipigwe—la wale walio mbinguni na wale walio duniani na wale walio chini ya ardhi^m— **11** na kila ulimi ukiri waziwazi kwamba Yesu Kristo ni Bwanaⁿ kwa utukufu wa Mungu Baba.

12 Kwa hiyo, wapendwa wangu, kama vile ambavyo mme kuwa mkatii sikuzote, si wakati tu ninapokuwapo, bali kwa utayari zaidi sasa nisi-pokuwapo, endeleeeni kuufanyia kazi wokovu wenu wenye-we kwa kuogopa na kutetemeka. **13** Kwa maana Mungu ndiye ambaye kwa mapenzi yake mema anawachochea, na kuwapa hamu na nguvu za kutenda. **14** Endeleeeni kufanya

2:3 *Au "unyenyeketu wa akili." 2:7 *Tnn., "na kuwa kama wanadamu." 2:8 *Tnn., "alipopatikana katika umbo la mwanadamu." #Angalia Kamusi, uku. 2012.

mambo yote bila kunung'u-nika^a wala kubishana,^b **15** ili mje kuwa bila lawama wala hatia, watoto wa Mungu^c wasio na dosari katikati ya kizazi kilicho kombo na kili-chopotoka,^d ambao kati yao mnaangaza kama mianga katika ulimwengu,^e **16** mkiendelea kulishika sana neno la uzima.^f Ndipo nitakuwa na sababu ya kushangilia katika siku ya Kristo, nikijua kwamba sikukimbia bure wala sikufanya kazi kwa bidii bure. **17** Hata hivyo, hata ikiwa ninamimnwa kama toleo la kinywaji^g juu ya dhabihu^h na utumishi mtakatifu* ambao imani yenu imewaongoza, ninafurahi na kushangilia pamoja nanyi nyote. **18** Vivyo hivyo, ninyi pia mnapaswa kufurahi na kushangilia pamoja nami.

19 Sasa ninatumaini katika Bwana Yesu kumtuma Timotheoⁱ kwenu upesi, ili nitiwe moyo nitakapopata habari kuwahusu ninyi. **20** Kwa maana sina mtu mwingine aliye na mwelekeo kama wake atakayejali kwa unyoofu mahangai-ko yenu. **21** Kwa maana wengine wote wanatafuta faida zao wenyewe, si za Yesu Kristo. **22** Lakini ninyi mnajua jinsi alivyojithibitisha mwenyewe, kwamba kama mtoto/na baba yake alitumikia pamoja nami katika kuendeleza habari njema. **23** Kwa hiyo, yeye ndiye ninayetumaini kumtuma mara tu nitakapoona jinsi mambo yangu yatakavyokuwa. **24** Kwa kweli, nina uhakika katika Bwana kwamba mimi mwenyewe pia nitakuja hivi karibuni.^k

2:17 *Au "utumishi wa watu wote."

SURA YA 2

a 1Ko 10:10
1Pe 4:9

b 1Ti 2:8

c Efe 5:1

d Kum 32:5

e Mt 5:14
Efe 5:8, 9
1Pe 2:9, 12

f Yoh 6:68
Ebr 4:12

g Hes 28:6, 7
2Ko 12:15
2Ti 4:6

h Ebr 13:15
1Pe 2:5

i 1Ko 4:17
1Ko 16:10

j 2Ti 1:2

k Flm 22

Safu ya 2

a Flp 4:18

b 1Ko 16:18
1Th 5:12, 13

c Flm 10, 13

SURA YA 3

d 2Ko 13:11
Flp 4:4
1Th 5:16

e Gal 5:2

f Yer 4:4
Ro 2:29
Kol 2:11

g Gal 6:14
Ebr 9:13, 14

25 Lakini sasa ninaona ni lazima nimtume kwenu Epafrodito, ndugu yangu na mfan-nyakazi mwenzangu na mwana-jeshi mwenzangu, na mju-mbe wenu na mtumishi wa kibinafsi kwa ajili ya uhitaji wangu,^a **26** kwa kuwa anatamani kuwaona ninyi nyote naye amehuzunika kwa sababu mlisikia alikuwa mgonjwa. **27** Kwa hakika, alikuwa mgonjwa karibu kufa; lakini Mungu alimhurumia. Kwa kweli, hakumhurumia yeye tu, bali mimi pia, ili nisipatwe na huzuni juu ya huzuni. **28** Kwa hiyo ninamtuma haraka bila kukawia, ili mtakapomwona, mshangilie tena, nami nipunguziwe wasiwasii. **29** Basi mkaribisheni kama ilivyo desturi katika Bwana kwa shangwe yote, nanyi mwendelee kuwaheshimu sana watu wa namna hiyo,^b **30** kwa kuwa alikaribia kufa kwa sababu ya kazi ya Kristo,^c akihatarisha uhai wake,^d ili ajazie kutokuwapo kwenu hapa kunitolea utumishi wa kibinafsi.^e

3 Mwishowe, ndugu zangu, endeleeni kushangilia katika Bwana.^d Sioni vibaya kuendelea kuwaandikia mambo yaleyale, na ni kwa ajili ya usalama wenu.

2 Jihadharini na mbwa; jihadharini na wale wanaosababisha madhara; jihadharini na wale wanaoukata mwili.^e

3 Kwa maana sisi ndio wenye tohara ya kweli,^f sisi tunao-tua utumishi mtakatifu kupitia roho ya Mungu na tunao-jisifu katika Kristo Yesu^g na ambao uhakika wetu haute-gemei mwili, **4** ingawa mimi

2:30 *Au labda, "kazi ya Bwana." #Au "akiihatarisha nafsi yake."

kati ya watu wote, nina sababu za kuwa na uhakika katika mwili.

Mtu yeyote akifikiri ana sababu za kuwa na uhakika katika mwili, mimi ninazo zaidi: **5** nilitahiriwa siku ya nane,^a mimi ni wa taifa la Israeli, wa kabila la Benjamini, Mwebrania aliyezaliwa kwa Waebrania;^b kuhusu sheria, Farisayo;^c **6** kuhusu bidii, nililitesa kutaniko;^d kuhusu uadilifu unaotegemea sheria, mtu ambaye hakuwa na hatia. **7** Lakini vitu vilivyokuwa faida kwangu, nimeviona kuwa hasara* kwa sababu ya Kristo.^e **8** Isitoshe, kwa kweli ninaviona vitu vyote kuwa hasara kwa sababu ya thamani bora zaidi ya kumjua Kristo Yesu Bwana wangu. Kwa ajili yake nimekubali hasara ya vitu vyote nami ninaviona kuwa takataka nyingi, ili niweze kumpata Kristo **9** nami nipatikane katika muungano naye, si kwa sababu ya uadilifu wangu mwenyewe, kwa kufuata Sheria, bali kwa sababu ya uadilifu kupitia imani^f katika Kristo,^g uadilifu unaoitoka kwa Mungu na unaotegemea imani.^h **10** Lengo langu ni kumjua yeye na nguvu za ufufuo wakeⁱ na kushiriki katika mateso yake,^j nikijitisha kwenye kifo kama chake,^k **11** ili kuona kama ikiwezekana nitaufikia ufufuo wa mape-ma kutoka kwa wafu.^l

12 Si kwamba tayari nime-lipokea au tayari nimefanywa kuwa mkamilifu, bali nina-ndeleva kujitahidi^m ili kuona kama pia ninaweza kulishika lile ambalo lilifanya Kristo

3:7 *Au labda, "nimeviacha kwa hiari."

SURA YA 3

a Mwa 17:12
Law 12:3

b 2Ko 11:22

c Mdo 23:6
Mdo 26:4, 5

d Mdo 8:3
Mdo 9:1, 2
Gal 1:13

e Mt 13:44

f Ro 4:5

g Gal 2:15, 16

h Ro 3:20-22

i 1Ko 15:22
2Ko 13:4

j Ro 8:17
2Ko 4:10
Kol 1:24

k Ro 6:5

l 1Th 4:16
Ufu 20:6

m Lu 13:24

Safu ya 2

a 1Ti 6:12

b Lu 9:62

c 1Ko 9:24

d 2Ti 4:8
Ebr 12:1

e Ebr 3:1

f 1Ko 14:20
Ebr 5:14

g 1Ko 4:16
2Th 3:9

h Ro 8:5
Yak 3:15

i Efe 2:19

j Yoh 18:36
Efe 2:6
Kol 3:1

k 1Ko 1:7
1Th 1:10
Tit 2:13
Ebr 9:28

l 1Ko 15:42, 49

Yesu anichague.*^a **13** Akina ndugu, sijioni kuwa tayari ni-melishika hilo; lakini jambo moja ni hakika: Ninayasa-hau mambo ya nyuma^b na ku-jinyoosha kuelekea mambo yaliyo mbele.^c **14** ninaendeleva kujitahidi kuelekea mra-di* kwa ajili ya tuzo^d ya mwito wa Mungu wa kwenda juu^e kupitia Kristo Yesu. **15** Kwa hiyo, wale walio wakomavu kati yetu^f na wawe na mta-zamo huu wa akili, na ikiwa mna mwelekeo wa akili ulio tofauti kwa njia yoyote, Mu-ngu atawafunulia mtazamo ulio hapo juu. **16** Kwa vyo-vyote, kwa kadiri ambavyo tu-mefanya maendeleo, na tue-ndeele kutembea kwa utarati-bu katika mwendo huohuo.

17 Kwa muungano, iweni waigaji wangu,^g akina ndugu, na mwendelee kuwaangalia wale wanaotembea katika njia inayopatana na mfano tuliowawekea. **18** Kwa maana kuna wengi—nilikuwa nikiwataja mara nyingi lakini sasa ninawataja pia nikilia—wanao-tembea kama adui za mti wa mateso* wa Kristo. **19** Mwisho wao ni uharibifu, na mungu wao ni tumbo lao, na utukufu wao kwa kweli ni aibu yao, na akili zao zinafikiria vitu vya duniani.^h **20** Lakinii uraia wetuⁱ uko mbinguni,^j nasi tunamsubiri kwa hamu mwokozi kutoka huko, Bwana Yesu Kristo,^k **21** ambaye ataugeuza mwili wetu wa hali ya chini uwe kama* mwili wake wenye utukufu^l kwa nguvu zake nyingi zinazomweze-

3:12 *Tnn., "ambalo aliliweka juu yangu." 3:14 *Au "lengo." 3:18 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 3:21 *Tnn., "ufanane na."

sha kuvitiisha vitu vyote kwa ke mwenyewe.^a

4 Kwa hiyo, ndugu zangu ninaowapenda na ninaotamani kuwaona, shangwe yangu na taji langu,^b simameni imara^c kwa njia hii katika Bwana, wapendwa wangu.

2 Ninawahimiza Euodia na Sintike wawe na akili moja katika Bwana.^d **3** Ndiyo, nina kuomba pia, ukiwa mfanyakazi mwenzangu wa kweli,^e uendelee kuwasaidia wanawake hao ambao wamejitahidi^f sana pamoja nami kwa ajili ya habari njema, pamoja na Klementi na vilevile wale wafanyakazi wenzangu wengine, ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima.^e

4 Shangilieni sikuzote katika Bwana. Nitasema tena, Shangilieni!^f **5** Usawaziko wenu^g na ujulikane kwa watu wote. Bwana yuko karibu. **6** Msihangaikie kuhusiana na jambo lolote,^h bali katika kila jambo kwa sala na dua pamoja na kutoa shukrani, mjulisheni Mungu maombi yenu;ⁱ **7** na amani^j ya Mungu inayozidi uelewaji wote itailinda mioyo yenu^k na nguvu zenu za akili* kupitia Kristo Yesu.

8 Mwishowe, akina ndugu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, mambo yoyote yaliyo ya hangaiko zito, mambo yoyote yaliyo ya uadilifu, mambo yoyote yaliyo safi kiadili, mambo yoyote yanayopendeka, mambo yoyote yanayosemwa vema, mambo yoyote ya wema wa adili, na mambo yoyote yanayostahili sifa, ende-

4:3 *Tnn., "mwenzangu kihalisi katika nira." #Au "wamepambana." 4:7 *Au "akili zenu; mawazo yenu."

SURA YA 3

a 1Ko 15:27
Ebr 2:8

SURA YA 4

b 1Th 2:19

c Flp 1:27

d Ro 15:5, 6
1Ko 1:10
2Ko 13:11
Flp 2:2
1Pe 3:8

e Zb 69:28
Lu 10:20

f Zb 64:10
1Th 5:16

g Tit 3:2
Yak 3:17

h Mt 6:25
Lu 12:22

i Yoh 16:23
Ro 12:12
1Pe 5:6, 7

j Yoh 16:33
Ro 5:1

k Kol 3:15

Safu ya 2

a Kol 3:2

b Flp 3:17

c 2Ko 11:8, 9

d 1Ti 6:6, 8
Ebr 13:5

e 1Ko 4:11
2Ko 6:4, 10
2Ko 11:27

f Isa 40:29
2Ko 4:7
2Ko 12:9, 10

g 2Ko 11:8, 9

leeni kuyafikiria* mambo hayo.^a **9** Mambo mliyofunza na vilevile mkayakubali na kuyasikia na kuyaona kuhusiana nami, mzoe kuyafanya hayo,^b na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.

10 Ninashangilia sana katika Bwana kwamba sasa mwishowe mmeanza tena kunihangaikia.^c Ingawa mlinihangaikia, hamkupata nafasi ya kuonyesha jambo hilo.

11 Sisemi hivyo kwa sababu nina uhitaji, kwa maana hata hali zangu ziweje nimejifunza kuridhika.^{*d} **12** Ninajua jinsi ya kupungukiwa na chakula,^e na jinsi ya kuwa na vitu vingi. Katika mambo yote na katika hali zote nimejifunza siri ya jinsi ya kushiba na pia jinsi ya kuwa na njaa, jinsi ya kuwa na wingi na pia jinsi ya kuisi bila kitu. **13** Kwa mambo yote nina nguvu kupitia yule anayenipa nguvu.^f

14 Hata hivyo, mlifanya vema kwa kushiriki pamoja nami katika dhiki yangu. **15** Kwa kweli, ninyi Wafilipi pia mnajua kwamba mwanzoni mlipojifunza habari njema, nilipoondoka Makedonia, hakuna kutaniko lililoshiriki pamoja nami katika kutoa na kupokea, isipokuwa ninyi peke yenu;^g **16** kwa maana nilipokuwa Thesalonike, mlinitumia kitu kwa ajili ya uhitaji wangu si mara moja tu bali mara mbili. **17** Si kwamba ninatafuta zawadi, bali ninataka zaidi linalowaletea faida zaidi kwenye akiba yenu. **18** Hata hivyo, nina kila kitu ninachohitaji, na hata zaidi. Nimejaziwa kila kitu, kwa

4:8 *Au "kuyatafakari." 4:11 *Au "kutosheka."

kuwa sasa nimepokea kutoka kwa Epafrodito^a vitu mlivyo-tuma, harufu tamu,^b dhabihu yenye kukubalika, inayompen-ndeza Mungu vema. **19** Naye Mungu wangu atawajazia ki-kamili uhitaji wenu^c kulinga-na na utajiri wake katika utukufu kupitia Kristo Yesu. **20** Sasa kwa Mungu na Baba yetu kuwe na utukufu milele na milele. Amina.

SURA YA 4

a Flp 2:25

b Kut 29:18

c 2Ko 9:8

Safu ya 2

a Flp 1:12,13

21 Mpeni kila mtakatifu sa-lamu zangu katika muunga-no na Kristo Yesu. Ndugu wa-lio pamoja nami wanawatu-mia salamu zao. **22** Wataka-tifu wote, lakini hasa wale wa nyumbani mwa Kaisari,^a wa-nawatumia salamu zao.

23 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana Yesu Kristo ziwe pa-moja na roho mnayoonyesha.

KWA

WAKOLOSAI

YALIYOMO

- | | |
|---|---|
| <p>1 Salamu (1, 2)
Shukrani kwa sababu ya imani ya Wakolosai (3-8)
Sala kwa ajili ya ukuzi wa kiroho (9-12)
Jukumu muhimu la Kristo (13-23)
Kazi ngumu ya Paulo kwa ajili ya kutaniko (24-29)</p> <p>2 Siri takatifu ya Mungu, Kristo (1-5)
Jihadharini na wadanganyifu (6-15)
Uhalisi ni wa Kristo (16-23)</p> | <p>3 Utu wa zamani na utu mpya (1-17)
Viueni viungo vya mwili wenu (5)
Upendo, kifungo kikamilifu cha muungano (14)
Ushauri kwa familia za Kikristo (18-25)</p> <p>4 Ushauri kwa mabwana (1)
“Dumuni katika sala” (2-4)
Kutembea kwa hekima kuelekea walio nje (5, 6)
Salamu za mwisho (7-18)</p> |
|---|---|

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kupitia mapenzi ya Mungu, na Timotheo^a ndugu yetu, **2** kwa watakatifu na ndugu waaminifu katika muungano na Kristo huko Kolosai:

Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu.

3 Sikuzote tunamshukuru Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, tunaposali kwa ajili yenu, **4** kwa kuwa tu-

SURA YA 1

a 1Ko 4:17

Safu ya 2

a 2Ti 4:8
1Pe 1:3, 4b Kol 1:23
1Ti 3:16

lisikia kuhusu imani yenu ka-tika Kristo Yesu na upendo mlio nao kwa watakatifu wote **5** kwa sababu ya tumaini mli-lowekewa akiba mbinguni.^a Hapo mwanzoni, mlisikia ku-husu tumaini hili kupitia uju-mbe wa kweli ya habari nje-ma **6** ambayo imekuja kwe-nu. Kama vile habari njema inavyozaa matunda na kuo-gezeka ulimwenguni kote,^b ndivyo pia inavyofanya mio-ngoni mwenu, tangu siku mli-

posikia na kujua kwa usahihi fadhili zisizostabiliwa za Mungu katika kweli. **7** Hivyo ndivyo mmejifunza kutoka kwa mtumwa mwenzetu mpendwa Epafra,^a ambaye ni mhudumu mwaminifu wa Kristo kwa ajili yetu. **8** Pia alitujulisha kuhusu upendo wenu katika njia ya kiroho.*

9 Hiyo ndiyo sababu pia tangu siku tuliposikia kuhusu jambo hilo, hatujaacha kamwe kusali kwa ajili yenu^b na kuomba mjazwe ujuzi sahihi^c wa mapenzi yake katika hekima yote na utambuzi wa kiroho,^d **10** na hivyo mtembee kwa kumstahili Yehova* ili kumpendeza kikamili mnapoendelea kuzaa matunda katika kila kazi njema na kuongezeka katika ujuzi sahihi wa Mungu;^e **11** nanyi mwimarishwe kwa nguvu zote kwa uwezo wake wenye utukufu^f ili mvumilie kikamili kwa subira na shangwe, **12** huku mkimshukuru Baba, aliyewafanya mstahili kushiriki urithi wa watakatifu^g katika nuru.

13 Alituokoa kutoka kwenye mamlaka ya giza^h na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wake mpendwa, **14** ambaye kupitia kwake tunaachiliwa huru kwa fidia, kusamehewa dhambi zetu.ⁱ **15** Yeye ndiye mfano wa Mungu asiyeonekana,^j mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote;^k **16** kwa sababu kupitia kwake vitu vingine vyote viliumbwa mbinguni na duniani, vitu vinyoonekana na vitu visi-

1:8 *Tnn., "katika roho." 1:10 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 1

a Kol 4:12,13
Flm 23

b Efe 1:15,16

c Flp 1:9

d 2Ti 2:7
1Yo 5:20

e Efe 1:17
2Pe 1:2

f Efe 3:14,16

g Ro 8:17
Efe 1:13,14

h Efe 2:1,2

i Efe 1:7

j Yoh 4:24
Yoh 10:30
Yoh 14:9
1Ti 1:17

k Ufu 3:14

Safu ya 2

a Yoh 1:3

b Yoh 1:10
Ebr 1:2

c Yoh 17:5

d Efe 1:22

e 1Ko 15:23
Ufu 1:5

f Kol 2:3,9

g 2Ko 5:19
Efe 1:10

h Law 17:11

i 1Ko 1:8

j Ufu 2:10

k 1Ko 3:11

l 1Ko 15:58
Ebr 3:14

m 1Ti 3:16

n Efe 3:8

vyoonekana,^a iwe ni viti vya ufalme au utawala au serikali au mamlaka. Vitu vingine vyote vimeumbwa kupitia kwake^b na kwa ajili yake. **17** Pia, yeye ni wa kabla ya vitu vingine vyote,^c na kupitia kwake vitu vingine vyote vilifanywa kuwapo, **18** naye ndiye kichwa cha mwili, kutaniko.^d Yeye ndiye mwanzo, mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu,^e ili awe wa kwanza katika mambo yote; **19** kwa sababu Mungu alipenda ujazo wote ukae ndani yake,^f **20** na kupitia yeye apatanishe kwake mwenyewe vitu vingine vyote^g kwa kufanya amani kupitia damu^h aliyomwaga juu ya mti wa mateso,^{*} iwe ni vitu vilivyo duniani au vitu vilivyo mbinguni.

21 Kwa kweli, ninyi ambao zamani mlikuwa mmetengwa, nanyi mlikuwa adui kwa sababu akili zenu zilikuwa zikifikiria matendo maovu, **22** sasa amewapatanisha tena kwa njia ya mwili wenye nyama wa huyo kupitia kifo chake, ili awatoe ninyi mkiwa watakatifu na wasio na dosari na bila shtaka lolote mbele zake!ⁱ **23** bora tu, bila shaka, mwendelee katika imani,^j mkiwekwa imara juu ya msingi^k na kuwa thabiti,^l bila kuondoshwa kwenye tumaini la habari njema mliyoisikia, na ambayo ilihubiriwa katika uumbaji wote chini ya mbingu.^m Mimi Paulo, nilikuja kuwa mhudumu wa hii habari njema.ⁿ

24 Ninashangilia sasa katika mateso yangu kwa ajili

1:20 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

yenu,^a nami ninakabili dhiki za Kristo ambazo bado hazimo katika mwili wangu kwa ajili ya mwili wake,^b ambao ni kutaniko.^c **25** Nilikuja kuwa mhudumu wa kutaniko hili kupatana na usimamizi^d kutoka kwa Mungu niliopewa kwa ajili yenu ili kulihubiri neno la Mungu kwa ukamili, **26** siri takatifu^e iliyokuwa imefichwa tangu mifumo ya mambo ili-yopita^{*f} na tangu vizazi vilivyopita. Lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake,^g **27** ambao Mungu amependewa kuwajulisha kati ya mataifa utajiri wenye utukufu wa hii siri takatifu,^h ambayo ni Kristo katika muungano nanyi, tumaini la utukufu wake.ⁱ **28** Yeye ndiye tunayemtanga, tukimwonya kila mtu na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, ili tumtoe kila mtu akiwa kamili katika muungano na Kristo.^j **29** Kwa kusudi hili kwa kweli ninafanya kazi kwa bidii, nikijikaza kwa uwezo wake unaotenda ndani yangu kwa nguvu.^k

2 Kwa maana ninataka mjue jinsi ninavyopambana sana kwa ajili yenu na kwa ajili ya wale walio huko Laodikia^l na kwa ajili ya wote ambao hawajaniona mimi binafsi.* **2** Ninafanya hivyo ili mioyo yao ifarijiwe^m na ili waunganishwe kwa upatano katika upendoⁿ na wawe na utajiri wote unaotokana na uhakikisho kamili wa uelewaji wao, ili wapate ujuzi sahihi wa siri takatifu ya Mungu, yaani, Kristo.^o

1:26 *Au "vizazi vya kale." Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:1 *Tnn., "hawajauona uso wangu katika mwili."

SURA YA 1

a Efe 3:1

b Mdo 9:16
Flp 3:10

c Efe 1:22, 23

d 1Ko 9:16, 17

e Efe 3:5-7
Efe 5:32f Lu 8:10
1Ko 2:7

g Ro 16:25, 26

h Efe 3:8, 9

i Ro 8:18

j Efe 4:13

k Flp 4:13

SURA YA 2

l Kol 4:16

m 2Ko 1:6

n Kol 3:14

o 1Ko 2:7
Efe 3:5, 6

Safu ya 2

a 1Ko 1:30
1Ko 2:16

b 1Ko 14:40

c 1Ko 15:58
Ebr 3:14d Efe 2:20
Efe 3:17

e Mt 7:24, 25

f Efe 5:20
1Th 5:18g Efe 5:6
Ebr 13:9

h Kol 1:19

i Efe 1:20, 21
1Pe 3:22

j Ro 6:6

k Ro 2:29
Flp 3:3

l Ro 6:4

m Efe 2:6
Kol 3:1n Mdo 2:24
Efe 1:19, 20

3 Hazina zote za hekima na za ujuzi zimefichwa kwa uangalifu ndani yake.^a **4** Nina-sema hivyo ili mtu yeyote asi-wadanganye kwa hoja zenye kushawishi. **5** Ingawa sipo katika mwili, nipo pamoja nanyi katika roho, nikishangilia kuona utaratibu wenu mzuri^b na uthabiti wa imani yenu katika Kristo.^c

6 Kwa hiyo, kama vile ambavyo mmempokea Kristo Yesu aliye Bwana, endeleeni kutembea katika muungano naye, **7** mkiwa mmetia mizizi na kujengwa katika yeye^d na kuimarisha katika imani,^e kama vile mliyofundishwa, mkijawa kabisa na shukrani.^f

8 Jihadharini ili mtu yeyote asiwachukue mateka* kupitia falsafa na udanganyifu^g mtupu kulingana na mapokeo ya wanadamu, kulingana na mambo ya msingi ya ulimwengu na si kulingana na Kristo; **9** kwa sababu ndani yake ujazozote wa sifa ya Mungu hu-kaa kimwili.^h **10** Basi mme-pata ujazo kupitia kwake, yule aliye kichwa cha serikali na mamlaka yote.ⁱ **11** Kwa uhusiano wenu pamoja naye, ninyi pia mlitahiriwa kwa tohara iliyofanywa bila mikono kwa kuuvua mwili wenye nyama,^j kwa tohara ambayo ni ya Kristo.^k **12** Kwa maana mlizikwa pamoja naye katika ubatizo wake,^l na kwa uhusiano wenu pamoja naye mli-fufuliwa^m pia pamoja kupitia imani yenu katika matendo yenye nguvu ya Mungu, ali-yemfufua Kristo kutoka kwa wafu.ⁿ

2:8 *Au "asiwachukue kama mawindo yake."

13 Zaidi ya hilo, ingawa mlikuwa wafu katika makosa yenu na katika hali ya kutotahiriwa ya mwili wenu, Mungu aliwafanya muwe hai pamoja naye.^a Alitusamehe kwa fadhili makosa yetu yote.^b **14** Na kuifuta* hati iliyoandikwa kwa mkono^c ambayo ilikuwa na amri^d na iliyokuwa ikitupinga.^e Ameiondoa njiani kwa kuipigilia misumari kwenye mti wa mateso.^{#f} **15** Na kupitia mti huo,* amezivua na kuziacha uchi serikali na mamlaka naye amezionyesha hadharani kwamba zimeshindwa,^g akiziongoza katika maandamano ya ushindi.

16 Kwa hiyo, msimruhusu mtu yeyote awahukumu kuhusu mnachokula na kunywa^h au kuhusu kushika sherehe au mwezi mpyaⁱ au sabato.^j **17** Mambo hayo ni kivuli cha mambo yanayokuja,^k bali uhalisi ni wa Kristo.^l **18** Msimruhusu mtu yeyote anayependewa na unyenyekevu wa uwongo na namna ya ibada ya malaika awanyang'anye tuzo,^m "akichukua msimamo juu ya"* mambo ambayo ameona. Kwa kweli, anajivuna bila sababu inayofaa kwa akili yake ya kimwili, **19** naye hashiki imara kichwa,ⁿ yeye ambaye kupitia kwake mwili wote huanjaliwa na kuunganishwa kwa upatano kupitia viungo na kano zake, na kufanywa ukue kwa ukuzi unaotoka kwa Mungu.^o

2:14 *Au "kuiondoa." #Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:15 *Au labda, "kupitia yeye." 2:18 *Yamenukuliwa kutoka kwenye desturi za mafumbo (jando) ya kipagani.

SURA YA 2

- a Efe 2:1, 5
b Mdo 2:38
c Kut 34:27
Kum 31:24-26
Ebr 7:18
d Efe 2:14, 15
e Ro 7:10
Gal 3:10
f Gal 3:13
Ebr 9:15
1Pe 2:24
g 1Yo 5:4
Ufu 3:21
h Ro 14:3, 17
i Zb 81:3
j Ro 14:6
k Ebr 8:5
Ebr 10:1
l Yoh 14:6
Ebr 9:11, 12
m Flp 3:14
n Efe 1:22, 23
o Efe 2:21
Efe 4:16

Safu ya 2

- a Gal 4:3
Kol 2:8
b Efe 2:15
Kol 2:14
c Mt 15:9
d 1Ti 4:3

SURA YA 3

- e Efe 2:6
f Zb 10:11
1Pe 3:22
g Flp 3:20
Flp 4:8
1Pe 1:13
h 1Yo 2:15
i Yoh 11:25
j 1Ko 15:42, 43
k Mk 9:43
Gal 5:24
l 1Ko 6:18
Efe 5:3

20 Ikiwa mlikufa pamoja na Kristo kuhusiana na mambo ya msingi ya ulimwengu,^a kwa nini mnaishi kana kwamba bado ninyi ni sehemu ya ulimwengu kwa kuendelea kujiitiisha chini ya amri hizi:^b **21** "Usishike, wala usionje, wala usiguse," **22** kuhusiana na mambo yote ambayo huangamia pamoja na matumizi yake, kulingana na amri na mafundisho ya wanadamu?^c **23** Ingawa mambo hayo huonekana kana kwamba yana hekima katika ibada ya kujituingia wenyewe na unyenyekevu wa uwongo, na kuute ndea mwili kwa ukali,^d hayana thamani yoyote katika kuzuia kuutosheleza mwili.

3 Hata hivyo, ikiwa mlifufuliwa pamoja na Kristo,^e endeeleni kutafuta mambo yaliyo juu, ambako Kristo ameketi kwenye mkono wa kuumwa wa Mungu.^f **2** Endeeleni kukaza akili zenu kwenye mambo yaliyo juu,^g si kwenye mambo yaliyo duniani.^h **3** Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika muungano na Mungu. **4** Wakati Kristo, aliye uhai wetu,ⁱ atakapofunuliwa, ndipo ninyi pia mtakapofunuliwa pamoja naye katika utukufu.^j

5 Kwa hiyo, viueni viungo vya mwili wenu^k vilivyvo duniani kuhusiana na uasherati,* uchafu, hamu isiyodhibitiwa ya ngono,^l tamaa yenye madhara, na pupa, ambayo ni ibada ya sanamu.

3:5 *Neno la Kigiriki *pornei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012.

6 Kwa sababu ya mambo hayo ghadhabu ya Mungu inakuja. 7 Hivyo ndivyo pia ninyi mlikuwa mkijiendesha* katika maisha yenu ya zamani.^{#a} 8 Lakini sasa, kwa kweli,^a lazima myaondoe mambo haya yote kutoka kwenu: ghadhabu, hasira, ubaya,^b matusi,^c na maneno machafu^d kutoka kinywani mwenu. 9 Msiambiane uwongo.^e Uvueni utu* wa zamani^f pamoja na mazoea yake, 10 na mjivike utu mpya,^g ambao kupitia ujuzi sahihi unafanywa kuwa mpya kulingana na mfano wa Yule aliyeuumba,^h 11 ambapo hakuna Mgiriki wala Myahudi, kutahiriwa wala kutohaririwa, mgeni, Msikithe,* mtumwa, au mtu huru; bali Kristo ni kila kitu na yumo katika vitu vyote.ⁱ

12 Basi, kama waliochaguliwa wa Mungu,^j watakatifu na wapendwa, jivikeni upendo mwororo wenye huruma,^k fadhili, unyenyekevu,^{*l} upole,^m na subira.ⁿ 13 Endeeleni kuvumiliana na kusameheana kwa hiari^o hata ikiwa yeyote ana sababu ya kulalamika juu ya mwingine.^p Kama vile Yehova* alivyowasamehe kwa hiari, nanyi lazima mfanye vivyo hivyo.^q 14 Lakini zaidi ya mambo haya yote, jivikeni upendo,^r kwa maana huo ni kifungo kikamilifu cha muungano.^s

15 Pia, acheni amani ya Kristo itawale mioyoni mwe-

3:7 *Au "mlikuwa mkitembea." #Au "mlipokuwa mkiishi hivyo." 3:9 *Tnn., "Mvueni mtu." 3:11 *Neno "Msikithe" lilimaanisha mtu asiye mstaarabu. 3:12 *Au "unyenyekevu wa akili." 3:13, 16, 22 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 3

a 1Ko 6:9-11
Efe 2:3
Tit 3:3

b 1Pe 2:1

c Efe 4:31

d Efe 5:3,4

e Efe 4:25
Ufu 21:28

f Efe 4:22

g Ro 12:2
Efe 4:24

h Mwa 1:26, 27
1Pe 1:16

i Gal 3:28

j 1Pe 2:9

k Flp 2:1, 2

l Ro 12:16

m Tit 3:2

n Efe 4:1, 2
1Th 5:14

o Met 19:11
Efe 4:32
1Pe 4:8

p Mt 18:15

q Mt 6:14
Mk 11:25

r 1Yo 3:23

s 1Ko 13:4-7

Safu ya 2

a Yoh 14:27
Flp 4:7

b 1Ko 14:26

c Efe 5:19

d 1Ko 10:31

e Efe 5:22
1Pe 3:1

f Efe 5:25
1Pe 3:7

g Efe 4:31

h Met 6:20
Lu 2:51
Efe 6:1

i Efe 6:4

j Efe 6:5, 6
Tit 2:9
1Pe 2:18

nu,^{*a} kwa maana ninyi, mliitwa kwenye amani hiyo katika mwili mmoja. Na mjionyeshe kuwa wenye shukrani. 16 Neno la Kristo na likae ndani yenu kwa wingi katika hekima yote. Endeeleni kufundishana na kutiana moyo[#] kwa zaburi,^b sifa kwa Mungu, nyimbo za kiroho zinazoimbwa kwa shukrani,[^] mkimwambia Yehova* mioyoni mwenu.^c 17 Jambo lolote mnalofanya kwa maneno au kwa matendo, fanyeni mambo yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kupitia kwake.^d

18 Enyi wake, jitiisheni kwa waume zenu,^e kwa kuwa inafaa katika Bwana. 19 Enyi waume, endeeleni kuwape nda wake zenu^f nanyi msiwakasirikie kwa uchungu.^{*g} 20 Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika kila jambo,^h kwa maana hilo humpendeza Bwana. 21 Enyi akina baba, msiwe mkiwakasirisha* watoto wenu,ⁱ ili wasivunjike moyo.[#] 22 Enyi watumwa, watiini katika kila jambo wale ambao ni mabwana wenu wanadamu,^{#j} si wakati tu wanapowatazama, ili tu kuwape ndeza wanadamu,[^] bali kwa unyoofu wa moyo, kwa kumwogopa Yehova.* 23 Lolote mnalofanya, lifanyeni kwa nafsi* yote kama kwa

3:15 *Au "idhibiti mioyo yenu." 3:16 #Au "kuonyana." ^Au "neema." 3:19 *Au "msiwe wakali kwao." 3:21 *Au "msiwachokoze; msiwaudhi." #Au "wasife moyo." 3:22 #Tnn., "kwa njia ya kimwili." ^Tnn., "si kwa matendo ya utumishi wa macho, kama wanaowape ndeza wanadamu." 3:23 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Nafsi."

Yehova,^a na si kwa wanadamu, **24** kwa maana mna-jua kwamba mtapokea kuto-ka kwa Yehova* urithi kama thawabu.^b Mtumikieni Bwana, Kristo. **25** Hakika yule anayetenda kosa atapokea mali-po kwa lile kosa alilote-nda,^c na hakuna ubaguzi wo-wote.^d

4 Enyi mabwana, watendeeni watumwa wenu kwa njia ya uadilifu na haki, mkijua kwamba ninyi pia mna Bwana mbinguni.^e

2 Dumuni katika sala,^f mki-kaa macho katika sala pamoja na kutoa shukrani.^g **3** Wakati huohuo, salini pia kwa ajili yetu,^h ili Mungu afungue mlan-gaze kwa ajili ya neno ili tutan-gaze siri takatifu kumhusu Kristo, ambayo kwa ajili yake nimefungwa gerezani,ⁱ **4** na ili niitangaze waziwazi kama ninavyopaswa.

5 Endeleeni kutembea kwa hekima kuelekea wale walio nje, mkitumia vizuri ka-bisa wakati wenu.*^j **6** Mane-no yenu na yawe yenye neema sikuzote,^k yaliyokolezwa chu-mvi, ili mjue jinsi mnavyopa-swa kumjibu kila mtu.^l

7 Tikiko,^m ndugu yangu mpendwa na mhudumu mwa-minifu na mtumwa mwenzan-gu katika Bwana, atawaam-bia habari zote kunihusu. **8** Ninamtuma kwenu ili mjue jinsi tunavyoendelea na ili aifariji mioyo yenu. **9** Ana-kuja pamoja na Onesimo,ⁿ ndugu yangu mwaminifu na mpendwa, ambaye anatoka kwenu; watawaambia kuhu-

3:23, 24 *Angalia Nyongeza A5. 4:5 *Tnn., "mkijinunulia wakati unaofaa."

SURA YA 3

a Lu 10:27
Ro 12:11

b Efe 6:8
1Pe 1:3, 4

c Ro 2:6
Gal 6:7

d Ro 2:11
1Pe 1:17

SURA YA 4

e Efe 6:9

f Lu 18:1
Ro 12:12
Efe 6:18

g Kol 3:15
1Th 5:18

h Ro 15:30

i Efe 6:19, 20
Flp 1:7

j Efe 5:15, 16

k Mt 5:13
Mk 9:50

l 1Pe 3:15

m Efe 6:21, 22

n Flm 10

Safu ya 2

a Mdo 19:29
Mdo 20:4
Mdo 27:2

b Mdo 12:12
Mdo 15:37
Flm 23, 24

c Ro 15:7

d Kol 1:7, 8

e Lu 1:3
Mdo 1:1

f Flm 23, 24

g Ro 16:5
1Ko 16:19

h 1Th 5:27

i Flm 1, 2

j 2Th 3:17

k Flp 1:7
Flm 9

su mambo yote yanayoende-lea huku.

10 Aristarko,^a mateka mwe-nzangu anawatumia salamu zake, na pia Marko,^b binamu ya Barnaba (ambaye mlipo-kea maagizo ya kumkaribisha^c ikiwa atakuja kwenu), **11** na Yesu anayelitwa Yusto, walio kati ya wale waliotahiriwa. Ni hawa tu walio wafanyaka-zi wenzangu kwa ajili ya Ufal-me wa Mungu, nao wameku-wa chanzo cha faraja* nyingi kwangu. **12** Epafra,^d mtu-mwa wa Kristo Yesu, ambaye ametoka kwenu, anawatumia salamu zake. Sikuzote anaji-kaza kwa ajili yenu katika sala zake, ili mwishowe msimame mkiwa kamili na kwa usadi-kisho imara katika mapenzi yote ya Mungu. **13** Kwa ma-na ninamtolea ushahidi kwa-mba anajitahidi sana kwa ajili yenu na kwa ajili ya wale walio Laodikia na Hierapoli.

14 Luka,^e daktari mpendwa anawatumia salamu zake, na pia Dema.^f **15** Wapeni sala-mu zangu ndugu huko Laodi-kia na pia msalimuni Nimfa na kutaniko lililo katika nyumba yake.^g **16** Na baada ya kuso-ma barua hii miongoni mwe-nu, pangeni isomwe^h pia kati-ka kutaniko la Walaodikia, nanyi pia msome ile ya kutoka Laodikia. **17** Pia, mwambie-ni Arkipo hivi:ⁱ "Zingatia hu-duma uliyoikubali katika Bwa-na, ili uitimize."

18 Hii ni salamu yangu, Paulo, kwa mkono wangu mwenyewe.^j Endeleeni kuku-mbuka vifungo vyangu vya ge-reza.^k Fadhili zisizostahiliwa ziwe pamoja nanyi.

4:11 *Au "msaada wa kunitia nguvu."

WATHESALONIKE

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Salamu (1)
Shukrani kwa ajili ya imani ya Wathesalonike (2-10)</p> <p>2 Huduma ya Paulo huko Thesalonike (1-12)
Wathesalonike walilikubali neno la Mungu (13-16)
Paulo atamani kuwaona Wathesalonike (17-20)</p> <p>3 Paulo asubiri ripoti kwa hamu akiwa Athene (1-5)
Ripoti ya Timotheo yenye kufariji (6-10)
Sala kwa ajili ya Wathesalonike (11-13)</p> | <p>4 Onyo dhidi ya uasherati (1-8)
Kupendana kikamili zaidi (9-12)
"Kushughulika na mambo yenu wenyewe" (11)
Waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza (13-18)</p> <p>5 Kuja kwa siku ya Yehova (1-5)
"Amani na usalama!" (3)
Kaeni macho, tunzeni akili zenu (6-11)
Himizo (12-24)
Salamu za mwisho (25-28)</p> |
|--|--|

1 Paulo, Silvano,^{*a} na Timotheo,^b kwa kutaniko la Wathesalonike walio katika muungano na Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo:

Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani.

2 Sikuzote tunamshukuru Mungu tunapowataja nyote katika sala zetu,^c **3** kwa maana tunaendelea kukumbuka kazi yenu ya uaminifu, kazi yenu ngumu ya upendo, na jinsi ambavyo mmevumilia kwa sababu ya tumaini lenu^d katika Bwana wetu Yesu Kristo mbele za Mungu, Baba yetu. **4** Akina ndugu, tunajua Mungu anawapenda na amewachagua, **5** kwa sababu hatukwahubiria habari njema kwa maneno tu, bali pia kwa nguvu na kwa roho takatifu na kwa usadikisho thabiti, kama mnavyojua jinsi tulivyot-

1:1 *Pia anaitwa Sila.

SURA YA 1

a Mdo 15:22
1Pe 5:12

b Mdo 16:1, 2

c 2Th 1:11, 12

d 1Pe 1:3, 4

Safu ya 2

a 1Ko 11:1
Flp 3:17
2Th 3:9

b 1Pe 2:21

c 1Th 2:14

d 2Th 1:4

e 1Ko 10:14
1Ko 12:2
Gal 4:8
1Yo 5:21

f Mdo 1:10, 11
Tit 2:13

tenda miongoni mwenu kwa ajili yenu. **6** Nanyi mlituiga sisi^a na Bwana pia,^b kwa kuwa mlilikubali neno kwa shangwe ya roho takatifu ingawa mlikuwa na dhiki nyingi,^c **7** na hivyo mkawa mfano mzuri kwa waamini wote katika Makedonia na Akaya.

8 Kwa kweli, mmelitangaza neno la Yehova* katika Makedonia na Akaya, na pia kila mahali watu wamesikia kuhusu imani yenu katika Mungu,^d hivi kwamba hatuhitaji kusema lolote. **9** Watu hao wanaendelea kusema jinsi tulivyowahubiria ninyi mara kwa kwanza na jinsi mlivyomgeukia Mungu na kuacha kuaбудu sanamu^e ili kumtumikia Mungu wa kweli aliye hai, **10** na kumsubiri Mwana wake aje kutoka mbinguni,^f ambaye alifufuliwa kutoka kwa wafu,

1:8 *Angalia Nyongeza A5.

yaani, Yesu, anayetukomboa kutoka kwenye ghadhabu inayoyukuja.^a

2 Kwa kweli, ninyi wenyewe akina ndugu mnajua kwa mba ziara yetu kwenu ilikuwa na mafanikio.^b **2** Kwa maana ingawa kwanza tulikuwa tumeteseka na kudharauliwa huko Filipi,^c kama mnavyojua, tulijipa ujasiri* kupitia Mungu wetu ili tuwatangazie ninyi habari njema ya Mungu^d licha ya upinzani.[#] **3** Kwa maana mambo tunayawahimiza hayatokani na kosa, ucha fu, wala udanganyifu, **4** lakini kwa kuwa tumekubaliwa na Mungu kukabidhiwa habari njema, hatusemi ili tuwape ndeze wanadamu, bali tumpendeze Mungu ambaye huchunguza mioyo yetu.^e

5 Kwa kweli, mnajua hatukutumia kamwe maneno ya kuwasifusifu au kuwa wanafiki tukiwa na makusudi yenye pupa;^f Mungu ni shahidi! **6** Wala hatujatafuta utukufu kutoka kwa wanadamu, iwe ni kutoka kwenu au kwa watu wengine, ingawa tukiwa mitume wa Kristo tungeweza kuwa mzigo wenye gharama kwenu.^g **7** Badala yake, tuliwatendea kwa upole, kama vile mama anayenyonyesha anavyowatunza* watoto wake kwa wororo. **8** Basi, kwa maana tulikuwa na upendo mwororo kwenu, tulijitahidi* kuwapa habari njema ya Mungu na hata uhai wetu[#] wenyewe,^h kwa sababu tuliwape nda sana.ⁱ

2:2 *Au "uhodari." #Au labda, "licha ya kupambana sana." 2:7 *Au "anavyowalea kwa upendo." 2:8 *Tnn., "tulipendezwa vema." #Au "nafsi zetu."

SURA YA 1

a 1Th 5:2
2Pe 3:12

SURA YA 2

b Mdo 17:1, 4

c Mdo 16:12
Mdo 16:22-24

d Mdo 17:1, 2

e Met 17:3
Yer 11:20

f Mdo 20:33

g 2Ko 11:9
2Th 3:8, 10

h Yoh 15:13

i Yoh 13:35

Safu ya 2

a Mdo 18:3
Mdo 20:34
2Ko 11:9
2Th 3:8, 10

b Mdo 20:31

c 1Ko 4:15

d Efe 4:1
Kol 1:10
1Pe 1:15

e Lu 22:28-30

f 1Pe 5:10

g 1Th 1:2, 3

h Mdo 17:5

i Mdo 2:22, 23
Mdo 7:52

j Mt 23:34

k Lu 11:52
Mdo 13:49, 50

l Ro 1:18

9 Hakika akina ndugu, mnakumbuka kazi yetu ngumu na yenye kutaabisha. Tuli fanya kazi usiku na mchana, ili tusimpe yeyote kati yenu mzigo wenye gharama,^a tuli powahubiria habari njema ya Mungu. **10** Ninyi ni mashahidi, na Mungu vilevile, wa jinsi tulivyokuwa washikamanifu na waadilifu na wasio laumika kwenu. **11** Mnajua jinsi tulivyoendelea kumhimiza, kumfariji, na kumshauri kila mmoja wenu,^b kama baba^c anavyowatendea watoto wake, **12** ili mwendelee kutembea kwa kumstahili Mungu^d anayewaita kwenye Ufalme^e na utukufu wake.^f

13 Kwa kweli, hii ndiyo sababu tunamshukuru Mungu bila kuacha,^g kwa kuwa mlipolipokea neno la Mungu, ambalo mlilisikia kutoka kwetu, mlilikubali si kama neno la wanadamu, bali kama lilivyo kwa kweli, neno la Mungu, ambalo pia linafanya kazi ndani yenu waamini. **14** Kwa maana, akina ndugu mliiga makutaniko ya Mungu yaliyo katika muungano na Kristo Yesu huko Yudea, kwa sababu mliteswa na wananchi wenzenu,^h kama vile wao pia wanavyoteswa na Wayahudi, **15** ambao hata walimuua Bwana Yesuⁱ na manabii na wakatutesa.^j Zaidi ya hayo, hawafanyi mambo yanayompendeza Mungu, na wanapinga mambo yanayowafaa wanadamu wote, **16** wakijaribu kutuzuia kuzungumza na watu wa mataifa ili waokolewe.^k Kwa hiyo, sikuzote wanajaza kipimo cha dhambi zao. Lakini hatimaye hasira yake imekuja juu yao.^l

17 Hata hivyo, akina ndu-
gu, tulipotenganishwa na-
nyu* kwa muda mfupi (kati-
ka mwili, bali si moyoni), kwa
kuwa tulitamani sana, tuli-
jitahidi kabisa kuwaona tena
uso kwa uso.[#] 18 Kwa sababu
hiyo, tulitaka kuja kwenu,
ndiyo, mimi Paulo, nilijaribu
si mara moja tu bali mara mbili;
lakini Shetani aliifunga njia
yetu. 19 Ni nini tumaini letu
au shangwe au taji la furaha
mbele ya Bwana wetu Yesu
wakati wa kuwapo kwake? Je,
kwa kweli si ninyi?^a 20 Kwa
kweli ninyi ndio utukufu na
shangwe yetu.

3 Basi tuliposhindwa kuvu-
milia, tuliamua kubaki
Athene peke yetu;^b 2 tuka-
mtuma Timotheo,^c ndugu yetu
na mhudumu wa Mungu* kati-
ka habari njema kuhusu Kri-
sto, ili awaimarishe[#] na
kuwafariji kuhusiana na imani
yenu, 3 ili yeyote asitiki-
swe* na dhiki hizo. Kwa
maana ninyi wenyewe mna-
jua hatuwezi kuepuka mate-
so hayo.^{#d} 4 Kwa kuwa tuli-
pokuwa pamoja nanyi, tuliku-
wa tukiwaambia mapema
kwamba tutapatwa na dhiki,
na imekuwa hivyo, kama mna-
vyojua.^e 5 Ndiyo sababu, ni-
liposhindwa kuvumilia hilo,
nilimtuma mtu ili nijue kuhu-
su uaminifu wenu,^f isiwe kwa-
mba Mjaribu^g alikuwa amewa-
jaribu na kazi yetu ngumu
ikawa ya bure.

6 Lakini Timotheo ameru-
di sasa hivi kutoka kwenu^h

2:17 *Au "tulipoachwa mayatima."
#Tnn., "kuona nyuso zenu." 3:2 *Au
labda, "mfanyakazi mwenzi wa Mungu."
#Au "awatie nguvu." 3:3 *Tnn., "asi-
yumbishwe." #Au "tumewekwa rasmi
kwa ajili ya hilo."

SURA YA 2

a 1Th 5:23
2Th 1:4

SURA YA 3

b Mdo 17:15

c Mdo 16:1, 2
Ro 16:21
1Ko 16:10

d Mdo 14:22
1Ko 4:9
1Pe 2:21

e 1Th 2:14

f 1Th 3:2

g Mt 4:3
2Ko 11:3

h Mdo 18:5

Safu ya 2

a 2Th 1:4

b 2Th 1:3

c 1Th 4:9
2Th 1:3

d 1Ko 1:8

e 1Th 2:19
1Th 5:23
2Th 2:1, 2

SURA YA 4

f Kol 1:10
1Pe 2:12

na kutujulisha habari njema
kuhusu uaminifu na upendo
wenu, kwamba mnaendelea
kutukumbuka kwa upendo na
kwamba mnatamani kutuo-
na kama sisi pia tunavyotama-
mani kuwaona. 7 Hiyo ndi-
yo sababu, katika taabu* na
dhiki zetu zote, tumefariji-
wa kwa sababu yenu na uami-
nifu mnaonyesha.^a 8 Kwa
sababu tunapata nguvu* iki-
wa mnasimama imara kati-
ka Bwana. 9 Kwa maana tu-
nawezaje kumshukuru Mungu
kwa ajili yenu kutokana na
shangwe kubwa tuliyo nayo
mbele za Mungu wetu kwa sa-
babu yenu? 10 Usiku na
mchana tunasali kwa bidii ka-
diri tunavyoweza ili tuwao-
ne uso kwa uso na kuongeza
chochote kilichopungua kati-
ka imani yenu.^b

11 Sasa Mungu Baba yetu
na Bwana wetu Yesu na wa-
tufungulie njia ili tuje kwe-
nu. 12 Zaidi ya hayo, Bwa-
na na awawezeshe mwongez-
zeke, ndiyo, mpendane zaidi^c
na kuwapenda wote, kama tu-
navyowapenda ninyi, 13 ili
afanye mioyo yenu kuwa ima-
ra, isiyolaumika katika uta-
katifu mbele za Mungu^d na
Baba yetu wakati wa kuwapo
kwa Bwana wetu Yesu^e pamo-
ja na watakatifu wake wote.

4 Mwishowe, akina ndugu,
kama tulivyowaagiza jinsi
mnavyopaswa kutembea ili
kumpendeza Mungu,^f kama
vile kwa kweli mnavyote-
mbea, tunawaomba na ku-
wahimiza katika Bwana Yesu
mwendelee kufanya hivyo kwa
ukamili zaidi. 2 Kwa maana

3:7 *Tnn., "uhitaji." 3:8 *Tnn., "tu-
naishi."

mnajua mwongozo tuliowapa* kupitia kwa Bwana Yesu.

3 Kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba mnapaswa kuwa watakatifu^a na mjepushe na uasherati.*^b **4** Kila mmoja wenu anapaswa kujua jinsi ya kuudhibiti mwili wake* mwenyewe^c katika utakatifu^d na heshima, **5** si kwa hamu yenye pupa ya ngono^e kama ya watu wa mataifa wasiomjua Mungu.^f **6** Mtu yeyote hapaswi kuvuka mipaka inayofaa na kumdhulumu ndugu yake katika jambo hilo, kwa sababu Yehova* ndiye hutoa adhabu kwa mambo yote haya, kama tulivyowaambia mapema na pia kuwaonya kwa uthabiti. **7** Kwa maana Mungu hakutuita tuishi maisha ya uchafu, bali tuwe watakatifu.^g **8** Kwa hiyo, mtu anayepuuza jambo hili, hampuuzi mwanadamu, bali Mungu,^h anayewapa ninyi roho yake takatifu.ⁱ

9 Hata hivyo, kuhusu upe-
ndo wa kindugu,^j hatuhitaji kuwaandikia ninyi, kwa maana ninyi wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana.^k **10** Kwa kweli, mwanatendea hivyo ndugu zenu wote katika Makedonia. Hata hivyo, tunawahimiza, akina ndugu, endeleeni kufanya hivyo kwa ukamili zaidi. **11** Muwe na lengo la kuishi kwa utulivu/na kushughulika na mambo yenu wenyewe^m na kufanya kazi kwa mikono yenu,ⁿ kama tulivyowaagiza, **12** ili mte-

4:2 *Au "maagizo tuliyowapa." 4:3 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 4:4 *Tnn., "chombo chake." 4:6, 15; 5:2 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 4

a Yoh 17:19
Efe 5:25-27
2Th 2:13
1Pe 1:15, 16

b Efe 5:3

c Kol 3:5
2Ti 2:22

d Ro 6:19

e 1Ko 6:18
Efe 5:5

f Zb 79:6
Efe 4:17, 19
1Pe 4:3

g Ebr 12:14
1Pe 1:15, 16

h 1Ko 6:18, 19

i 1Yo 3:24

j Ro 12:10

k Yoh 13:34, 35
1Pe 1:22
1Yo 4:21

l 2Th 3:11, 12

m 1Pe 4:15

n 1Ko 4:11, 12
Efe 4:28
2Th 3:10
1Ti 5:8

Safu ya 2

a Ro 12:17

b Yoh 11:11
Mdo 7:59, 60
1Ko 15:6

c 1Ko 15:32

d Ro 14:9
1Ko 15:3, 4

e 1Ko 15:22, 23
Flp 3:20, 21
2Th 2:1
Ufu 20:4

f Yud 9

g 1Ko 15:51, 52

h Mdo 1:9

i 2Th 2:1

j Yoh 14:3
Yoh 17:24
2Ko 5:8
Flp 1:23
Ufu 20:6

SURA YA 5

k Sef 1:14

l Mt 24:36
2Pe 3:10

1 WATHESALONIKE 4:3-5:3

mbee kwa adabu machoni pa watu walio nje^a na msipungu-kiwe chochote.

13 Zaidi ya hayo, akina ndugu, tunataka mwelewe* kuhusu wale wanaolala usingizi katika kifo,^b ili msihuzunike kama wanavyofanya watu wasio na tumaini.^c

14 Kwa maana ikiwa tunaa-
mini kwamba Yesu alikufa na kufufuliwa,^d vivyo hivyo Mungu atawafufua wale ambao wamelala usingizi katika kifo kupitia Yesu.^e **15** Kwa maana tunawaambia hivi kwa neno la Yehova,* kwamba sisi tulio hai ambao tutabaki mpaka kuwapo kwa Bwana hatawatangulia kwa vyovyote wale ambao wamelala usingizi katika kifo; **16** kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni akiwa na mwito wenye amri, kwa sauti ya malaika mkuu^f na tarumbeta ya Mungu, na wale waliokufa katika muungano na Kristo watafufuliwa kwanzwa.^g **17** Baadaye, sisi tulio hai ambao tumebaki, tunityakuliwa pamoja nao katika mawingu^h ili tukutane na Bwanaⁱ hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana sikuzote.^j **18** Kwa hiyo endeleeni kufarijiana kwa maneno hayo.

5 Sasa akina ndugu, hamhitaji kuandikiwa chochote kuhusu nyakati na majira. **2** Kwa maana ninyi wenyewe mnajua vema kwamba siku ya Yehova*^k inakuja kama vile mwizi anavyokuja usiku.^l

3 Wakati watakapokuwa wakisema: "Amani na usalama!"

4:13 *Au "msikose kujua."

ndipo uharibifu wa ghafla utakapowapata mara moja,^a kama vile maumivu ya kuzaa ya mwanamke mwenye mimba, nao hawataponyoka kamwe. **4** Lakini ninyi, akina ndugu, hamko gizani, hivi kwamba siku hiyo iwafikie ghafla kama vile ingewafikia wezi, **5** kwa maana ninyi nyote ni wana wa nuru na wana wa mchana.^b Sisi si wa usiku wala wa giza.^c

6 Basi, tusiendelee kulala usingizi kama wengine wanavyofanya,^d bali tukae macho^e na kutunza akili zetu.^f **7** Kwa maana wale wanaolala usingizi hulala usiku, na wale wanaolewa, hulewa usiku.^g **8** Lakini sisi tulio wa mchana, na tutunze akili zetu na kuvaa bamba la kifua ni imani na upendo na tumaini la wokovu kama kofia ya chuma^h **9** kwa sababu Mungu hakutuchagua ili tupatwe na hasira, bali tupate wokovuⁱ kupitia Bwana wetu Yesu Kristo. **10** Alikufa kwa ajili yetu,^j ili kama tuko macho au tumelala usingizi,^{*} tuishi pamoja naye.^k **11** Kwa hiyo endeleeni kutiana moyo^{*} na kujengana,^l kama vile kwa kweli nnavyofanya.

12 Sasa tunawaomba, akina ndugu, waheshimuni wale wanaofanya kazi kwa bidii miongoni mwenu na wanao-wasimamia katika Bwana na kuwaonya ninyi; **13** na mwafikirie kwa njia inayozidi ile ya kawaida katika upendo kwa sababu ya kazi yao.^m Dumisheni amani miongoni mwenu.ⁿ **14** Kwa upande mwingi-

5:10 *Au "tumelala usingizi katika kifo."
5:11 *Au "kufarijiana."

SURA YA 5

a Zb 37:10
Yer 8:11

b Yoh 12:36
Ro 13:12
Efe 5:8

c Yoh 8:12
Kol 1:13
1Pe 2:9

d Ro 13:11

e Mt 24:42

f 1Pe 5:8

g Ro 13:13

h Efe 6:14-17

i 2Th 2:13

j Ro 5:8

k 1Th 4:16,17

l Ro 1:11,12
Ro 15:2

m Flp 2:29,30
1Ti 5:17
Ebr 13:7

n Mk 9:50
2Ko 13:11

Safu ya 2

a Law 19:17
2Ti 4:2

b 1Ko 13:4
Gal 5:22
Efe 4:1,2
Kol 3:13

c Mt 5:39

d Ro 12:17,19

e 2Ko 6:4,10
Flp 4:4

f Lu 18:1
Ro 12:12

g Efe 5:20
Kol 3:17

h Efe 4:30

i 1Ko 14:1

j 1Yo 4:1

k Ayu 2:3

l 1Ko 1:8

m Ro 15:30

n Kol 4:16

ne, tunawahimiza akina ndugu, waonyeni* wale wasiofua-ta utaratibu,^a wafarijini wale walioshuka moyo,^b wasaidieni walio dhaifu, iweni na subira kwa watu wote.^b **15** Hakikisheni hakuna yeyote anayelipa ubaya kwa ubaya,^c bali sikuzote mwendelee kutendea-na mema kati yenu na kwa wengine wote.^d

16 Shangilieni sikuzote.^e **17** Salini bila kuacha.^f **18** Toeni shukrani kuhusu kila jambo.^g Hayo ndiyo mape-nzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu. **19** Msiuzime moto wa roho.^h **20** Msi-tendee unabii kwa dharau.ⁱ **21** Hakikisheni mambo yote;^j shikamaneni na yaliyo mema. **22** Epukeni kila aina ya uovu.^k

23 Mungu wa amani na awatakase kikamili. Na bila kasoro yoyote, roho na nafsi* na mwili wenu akina ndugu, na vihifadhiwe bila lawama wakati wa kuwapo kwa Bwana wetu Yesu Kristo.^l **24** Yule anayewaita ninyi ni mwaminifu, na kwa hakika atafanya hivyo.

25 Akina ndugu, endeleeni kusali kwa ajili yetu.^m

26 Wasalimuni ndugu wote kwa busu takatifu.

27 Ninawaweka chini ya wajibu mzito kwa Bwana mha-kikishe kwamba ndugu wote wanasomewa barua hii.ⁿ

28 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana wetu Yesu Kristo ziwe pamoja nanyi.

5:14 *Au "mwakaripie." ^aAu "wale walio-vunjika moyo." Tnn., "wale walio na nafsi ndogo." 5:23 *Au "uhai." Angalia Kamusi, uku. 2012.

WATHESALONIKE

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Salamu (1, 2)
Imani ya Wathesalonike yazidi kukua (3-5)
Kisasi dhidi ya wasiotii (6-10)
Sala kwa ajili ya kutaniko (11, 12)</p> | <p>2 Yule mtu wa uasi-sheria (1-12)
Wahimizwa kubaki imara (13-17)</p> <p>3 Endeeleni kusali (1-5)
Onyo dhidi ya kutofuata utaratibu (6-15)
Salamu za mwisho (16-18)</p> |
|--|--|

1 Paulo, Silvano,* na Timotheo,^a kwa kutaniko la Wathesalonike katika muungano na Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo:

2 Na muwe na fadhili zizozostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo.

3 Tuna wajibu wa kumshukuru Mungu sikuzote kwa sababu yenu, akina ndugu. Hilo linafaa kwa kuwa imani yenu inakua sana na upendo wa kila mmoja wenu unaongezeka kati yenu.^b **4** Ndiyo maana tunajivunia ninyi^c kati ya makutaniko ya Mungu kwa sababu ya uvumilivu na imani yenu katika mateso yenu yote na taabu* mnayopata.^{#d} **5** Huu ni uthibitisho wa hukumu ya uadilifu ya Mungu, inayowaongoza kuhesabiwa kuwa mnastahili Ufalme wa Mungu, ambao kwa kweli mnateseka kwa ajili yake.^e

6 Hii inazingatia kwamba ni jambo la uadilifu kwa Mungu kuwalipa dhiki wale wanaowasababishia ninyi dhiki.^f **7** Lakini ninyi mnaopa-

1:1 *Pia anaitwa Sila. 1:4 *Au "dhiki."
#Au "mnayovumilia."

SURA YA 1

a 2Ko 1:19

b 1Th 3:12
1Th 4:9,10

c 1Th 2:19

d 1Th 1:6
1Th 2:14
1Pe 2:21

e Mdo 14:22
Ro 8:17
2Ti 2:12

f Ro 12:19
Ufu 6:9,10

Safu ya 2

a Lu 17:29,30
1Pe 1:7

b Mk 8:38

c Ro 2:8

d 2Pe 3:7

e Ro 8:30

ta dhiki mtapata kitulizo pamoja nasi wakati wa ufunuo wa Bwana Yesu^a kutoka mbinguni akiwa pamoja na malika wake wenye nguvu^b **8** katika mwali wa moto, atakapoleta kisasi juu ya wale wasiotii habari njema na wale wasiotii habari njema kumhusu Bwana wetu Yesu.^c **9** Watu hao watapata hukumu ya adhabu ya uharibifu wa milele^d kutoka mbele za Bwana na kutoka kwa utukufu wa nguvu zake, **10** wakati atakapokuja kutukuzwa kuhusiana na watakatifu wake na kustaajabiwa siku hiyo kati ya wote walioonyesha imani, kwa sababu ushahidi tuliotoa ulikubaliwa kwa imani kati yenu.

11 Kwa hiyo, tunasali sikuzote kwa ajili yenu, kwamba Mungu wetu awahesabu kuwa mnastahili mwito wake^e na kwa nguvu zake kufanya kika-mili mambo yote yanayompendeza na kila kazi ya imani. **12** Ili jina la Bwana wetu Yesu litukuzwe ndani yenu nanyi katika muungano naye, kulingana na fadhili zizozostahiliwa za Mungu wetu na za Bwana Yesu Kristo.

2 Hata hivyo, akina ndugu, kuhusu kuwapo kwa Bwana wetu Yesu Kristo^a na kukusanywa kwetu pamoja kwake,^b tunawaomba **2** msitikiwe upesi kutoka kwenye kufikiri kwenu wala msitishwe na maneno yaliyoongozwa na roho^{*c} au ujumbe uliosembwa au barua inayodhaniwa kutoka kwetu, kwamba siku ya Yehova^{#d} imefika.

3 Msiruhusu mtu yeyote awapotoshe^{*} kwa njia yoyote, kwa sababu siku hiyo haitafika kabla uasi imani^e haujatokea kwanza na yule mtu wa uasi sheria^f kufunuliwa, mwana wa maangamizi.^g **4** Yeye ni mpinzani na hujiinua juu ya wale wanaoitwa mungu au vitu vinavyoabudiwa,^{*} na hivyo huketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha waziwazi kuwa mungu. **5** Je, hamkumbuki kwamba nilikuwa nikiwaambia mambo hayo nilipokuwa pamoja nanyi?

6 Sasa mnajua kinachozuia, ili afunuliwe wakati wake unaofaa. **7** Kwa kweli, fumbo la uasi sheria huu tayari linafanya kazi,^h lakini ni mpaka tu yule anayeuzaia sasa atakapoondolewa. **8** Ndipo, kwa kweli, yule mwasi sheria atafunuliwa, ambaye Bwana Yesu atamwangamiza kwa roho ya kinywa chake/ na kumharibu kupitia ufunuo/ wa kuwapo kwake. **9** Lakini kuwapo kwa huyo mwasi sheria ni kupitia kazi ya Shetani^k pamoja na kila tendo lenye nguvu na ishara za uwongo na

2:2 *Au "kupitia kwa roho." Angalia Kamusi, uku. 2012, "Roho." 2:2, 13; 3:1 *Angalia Nyongeza A5. 2:3 *Au "awashawishi." 2:4 *Au "vinavyohe-shimiwa."

SURA YA 2

- a Mt 24:3
b 1Th 4:17
c 1Yo 4:1
d Sef 1:14
2Pe 3:10
e 1Ti 4:1
2Ti 2:16-18
2Ti 4:3
2Pe 2:1
1Yo 2:18, 19
f Mt 7:15
Mdo 20:29, 30
g 2Pe 2:1, 3
h Mdo 20:29, 30
1Ko 11:18, 19
1Yo 2:18
i Isa 11:4
Ufu 19:15
j 1Ti 6:13-15
2Ti 4:1, 8
k 2Ko 11:3

Safu ya 2

- a Mt 24:24
b Mt 24:11
c Mt 24:5
1Ti 4:1
2Ti 4:3, 4
d Yoh 6:44
Ro 8:30
e Yoh 17:17
1Ko 6:11
1Th 4:7
f 1Pe 5:10
g 1Ko 15:58
1Ko 16:13
h 1Ko 11:2
i 1Yo 4:10
j 1Pe 1:3, 4

SURA YA 3

- k Ro 15:30
1Th 5:25
Ebr 13:18
l Mdo 19:20
1Th 1:8
m Isa 25:4
n Mdo 28:24
Ro 10:16

mambo ya ajabu^{*a} **10** na kila namna ya udanganyifu usio wa uadilifu^b kwa wale wanaoangamia, kama malipo kwa sababu hawakukubali kuipenda kweli ili waokolewe. **11** Ndiyo sababu Mungu anaacha wapotoshwe kupitia udanganyifu, na hivyo waamini uwongo,^c **12** ili wote wahukumiwe kwa sababu hawakuamini kweli, bali walipenda ukosefu wa uadilifu.

13 Hata hivyo, tuna wajiibu wa kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu akina ndugu mnaopendwa na Yehova,[#] kwa sababu tangu mwanzo Mungu aliwachagua^d ili mwokolewe kwa kuwatakasae^e kupitia roho yake na imani yenu katika kweli. **14** Aliwaita kupitia habari njema tunayotangaza, ili mpate utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo.^f **15** Basi, akina ndugu, simameni imara^g na mwendeele kufuata desturi mli-zofundishwa,^h iwe ni kupitia ujumbe wa maneno au barua kutoka kwetu. **16** Zaidi ya hayo, Bwana wetu Yesu Kristo, na Mungu Baba yetu aliyetupendaⁱ na kutupatia faraja ya milele na tumaini jema/^j kupitia fadhili zisizostahiliwa, **17** na aifairiji mioyo yenu na kuwaimarisha^{*} katika kila tendo na neno jema.

3 Mwishowe, akina ndugu, endeleeni kusali kwa ajili yetu,^k ili neno la Yehova[#] lizidi kuenea upesi/^l na kutukuzwa, kama ilivyo kwenu, **2** na kwamba tukombolewe kutoka kwa watu hatari na waovu,^m kwa maana imani si mali ya watu wote.ⁿ **3** Laki-

2:9 *Au "miujiza." 2:17 *Au "kuwatia nguvu."

ni Bwana ni mwaminifu, naye atawaimarisha na kuwalinda dhidi ya yule mwovu. **4** Zaidi ya hayo, tuna uhakika katika Bwana kuwahusu ninyi, kwamba mnafanya na mtaendelea kufanya mambo tunayowaagiza. **5** Bwana na aendelee kuongoza mioyo yenu ili mfanikiwe kumpenda Mungu^a na kuvumilia^b kwa ajili ya Kristo.

6 Sasa akina ndugu, tuna-waagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo, mjepushe na kila ndugu asiyefuata utaratibu^c na desturi* mlizopokea[#] kuto-ka kwetu.^d **7** Kwa maana ninyi wenyewe mnajua jinsi mnavyopaswa kutuiga,^e kwa sababu hatukukosa kufuata utaratibu tulipokuwa nanyi, **8** wala hatukula chakula cha yeyote bure. ^{*f} Badala yake, tulifanya kazi ngumu na yenye kutaabisha usiku na mchana ili tusimpe yeyote kati yenu mzigo wenye gharama.^g **9** Si kwamba hatuna mamlaka,^h bali tulitaka kuwawekea mfan-ano ili mtuige.ⁱ **10** Kwa kwe-li, tulipokuwa nanyi tulikuwa

3:6 *Au "maagizo." [#]Au labda, "walizopokea." 3:8 *Au "bila kulipa."

SURA YA 3

a 1Yo 5:3

b Lu 21:19
Ro 5:3

c 1Th 5:14

d 1Ko 11:2
2Th 2:15
2Th 3:14e 1Ko 4:16
1Th 1:6

f Mdo 20:34

g Mdo 18:3
1Ko 9:14, 15
2Ko 11:9
1Th 2:9h Mt 10:9, 10
1Ko 9:6, 7i 1Ko 11:1
Flp 3:17

Safu ya 2

a 1Th 4:11, 12
1Ti 5:8

b 1Th 5:14

c 1Ti 5:13
1Pe 4:15

d Efe 4:28

e 2Th 3:6

f 1Th 5:14

g Joh 14:27

h 1Ko 16:21
Kol 4:18

tukiwaagiza hivi: "Mtu yeyote asiyetaka kufanya kazi, asile chakula."^a **11** Kwa maana tunasikia watu fulani miongoni mwenu hawafuati utaratibu,^b hawafanyi kazi yoyote, bali wanajiingiza katika mambo ya-siyowahusu.^c **12** Tunawaagiza watu hao na kuwahimiza katika Bwana Yesu Kristo wafanye kazi kwa utulivu na kula chakula ambacho wao wenyewe wamekifanyia kazi.^d

13 Nanyi akina ndugu, msichoke kutenda mema. **14** Lakini ikiwa yeyote hatii maneno yetu kupitia barua hii, mtieni alama na mwache kushirikiana naye,^e ili aone aibu. **15** Lakini msimwone mtu huyo kama adui, bali endeeleni kumwonya^f kama ndugu.

16 Basi, Bwana wa amani na aendelee kuwapa amani kwa kila njia.^g Bwana awe nanyi nyote.

17 Hii ni salamu yangu, mimi Paulo, kwa mkono wangu mwenyewe,^h ambayo ni ishara katika kila barua; hivi ndivyo ninavyoandika.

18 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana wetu Yesu Kristo na zive pamoja nanyi nyote.

BARUA YA KWANZA KWA

TIMOTHEO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1, 2)
Onyo dhidi ya walimu wa uwongo (3-11)
Paulo atendewa kwa fadhili zisizostahiliwa (12-16)
Mfalme wa umilele (17)
'Pigana vita vizuri' (18-20)

- 2 Kusali kwa ajili ya watu wa namna zote (1-7)
Mungu mmoja, mpatanishi mmoja (5)
Fidia inayolingana kwa ajili ya wote (6)

- Maagizo kwa wanaume na wanawake (8-15)
Kuvaa kwa kiasi (9, 10)
- 3 Sifa za kustahili kuwa waangalizi (1-7)
Sifa za kustahili kuwa watumishi wa huduma (8-13)
Siri takatifu ya ujitoaji-kimungu (14-16)
- 4 Onyo dhidi ya mafundisho ya roho waovu (1-5)
Jinsi ya kuwa mhudumu mzuri wa Kristo (6-10)
Tofauti kati ya mazoezi ya kimwili na ujitoaji-kimungu (8)
Angalia kufundisha kwako (11-16)
- 5 Jinsi ya kuwatendea vijana na wazee (1, 2)

- Kuwasaidia wajane (3-16)
Kuandaa mahitaji ya watu wa nyumba yako (8)
- Kuheshimu wazee wenye bidii (17-25)
"Divai kidogo kwa ajili ya tumbo lako" (23)
- 6 Watumwa wawaheshimu mabwana wao (1, 2)
Walimu wa uwongo na kupenda pesa (3-10)
Maagizo kwa ajili ya mtu wa Mungu (11-16)
Kuwa tajiri katika matendo mema (17-19)
Linda mambo uliyokabidhiwa (20, 21)

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na ya Kristo Yesu, tumaini letu,^a **2** kwa Timotheo,^{*b} mwanangu halisi^c katika imani:

Na uwe na fadhili zisizostahiliwa, rehema, na amani kutoka kwa Mungu Baba na Kristo Yesu Bwana wetu.

3 Kama nilivyokutia moyo ubaki Efeso nilipokuwa karibu kwenda Makedonia, sasa ninakutia moyo ufanye vivyo hivyo, ili uwaamuru watu fulani wasifundishe mambo tofauti, **4** wala kusikiliza hadithi za uwongo^d na kuchunguzachunguza ukoo. Mambo hayo hayaleti manufaa yoyote^e bali hutokeza maswali badala ya kuleta chochote kutoka kwa Mungu kuhusiana na imani. **5** Kwa kweli, kusudi la agizo hili^{*f} ni upendo^f unaotokana na moyo safi na dhambi njema na imani^g bila unafi-

1:2 *Maana yake "Mtu Anayemheshimu Mungu." 1:5 *Au "mamlaka hii; amri hii."

SURA YA 1

a 1Pe 1:3, 4

b Mdo 16:1, 2
Flp 2:19, 20

c 1Ko 4:17

d 1Ti 4:7
2Ti 4:3, 4
Tit 1:13, 14e 1Ti 6:20
2Ti 2:14

f Ro 13:8

g Gal 5:6

Safu ya 2

a 1Ti 6:20
2Ti 2:16-18

b Yak 3:1

c Gal 3:19

ki. **6** Kwa kuyaacha mambo hayo, watu fulani wameke-
ngeushwa na kujiingiza katika
mazungumzo yasiyo na ma-
na.^a **7** Wanataka kuwa wali-
mu^b wa sheria, lakini hawae-
lewi mambo wanayosema au
mambo wanayosisitiza sana.

8 Sasa tunajua kwamba
Sheria ni nzuri ikiwa mtu anai-
tumia vizuri,^{*} **9** na tunata-
mbua kwamba sheria haiwe-
kwi kwa ajili ya mtu mwadili-
fu, bali kwa ajili ya watu
wanaovunja sheria^c na waa-
si, watu wasiomwogopa Mu-
ngu na watenda dhambi, wasio
washikamanifu^{*} na wasio-
heshimu mambo matakatifu,
wale wanaoua akina baba, aki-
na mama, au watu wengine,
10 waasherati,^{*} wanaume wa-
naofanya ngono na wanaume,[#]
wateka nyara, waongo, wanao-
toa ushahidi wa uwongo,^Δ na

1:8 *Tnn., "kisheria." 1:9 *Au "wasio na upendo mshikamanifu." 1:10 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Uasherati." #Tnn., "wanaume wanaoalala na wanaume." ΔAu "wanaoapa kwa uwongo."

jambo lingine lolote ambalo ni kinyume cha fundisho lenye manufaa*^a **11** kulingana na habari njema yenye utukufu ya Mungu mwenye furaha, ambayo nilikabidhiwa.^b

12 Ninamshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu, kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu kwa kunipa huduma,^c **13** ingawa zamani nilikuwa mkufuru na mtesaji na mtu mwenye dharau.^d Hata hivyo, nilionyeshwa rehema, kwa sababu nilitenda bila ujuzi na sikuwa na imani. **14** Lakini fadhili zisizostahiliwa za Bwana wetu zilizidi sana pamoja na imani na upendo ulio katika Kristo Yesu. **15** Maneno haya ni yenye kuaminika na yanastahili kukubaliwa kabisa: Kristo Yesu alikuja ulimwenguni ili kuwaokoa watenda dhambi.^e Kati yao, mimi ndiye wa kwanza kabisa.^f **16** Hata hivyo, nilionyeshwa rehema ili kupitia mimi nikiwa wa kwanza kabisa, Kristo Yesu aonyeshe subira yake yote, nami niwe mfanano kwa wote watakaomwamini ili kupata uzima wa milele.^g **17** Sasa kwa Mfalme wa umilele,^h asiyeweza kuharibikaⁱ na asiyeonekana,^j Mungu pekee,^k kuwe na heshima na utukufu milele na milele. Amina.

18 Mwanangu Timotheo, ninakukabidhi agizo hili,^{*} ili kulingana na unabii uliotolewa kukuhusu, uendelee kupigana vita vizuri,^l **19** ukishika imani na dhamiri njema,^m ambayo wengine wameitupilia mbali na hivyo imani yao ikavunjika.

1:10 *Au "lenye afya; lenye faida." 1:18 *Au "mamlaka hii; amri hii."

SURA YA 1

a 2Ti 1:13
Tit 1:7,9
b Gal 2:7,8
c Mdo 9:15
2Ko 3:5,6
d Mdo 8:3
Mdo 9:1,2
Gal 1:13
Flp 3:5,6
e Lu 5:32
2Ko 5:19
1Yo 2:1,2
f Mdo 9:1,2
1Ko 15:9
g Yoh 6:40
Yoh 20:31
h Zb 10:16
Zb 90:2
Da 6:26
Ufu 15:3
i Ro 1:23
j Kol 1:15
k Isa 43:10
1Ko 8:4
l 2Ti 2:3
m 1Ti 1:5

Safu ya 2

a 2Ti 2:16-18
b 1Ko 5:5,11

SURA YA 2

c Mt 5:44
d Yer 29:7
e Yud 25
f Isa 45:22
Mdo 17:30
Ro 5:18
1Ti 4:10
g Kum 6:4
Ro 3:30
h Ebr 8:6
Ebr 9:15
i 1Ko 11:25
j Mdo 4:12
Ro 5:15
2Ti 1:9,10
k Mt 20:28
Mk 10:45
Kol 1:13,14
l Mdo 9:15
m Gal 2:7,8
n Gal 1:15,16
o Zb 141:2
p Yak 1:20
q Flp 2:14

20 Himenayo^a na Aleksanda ni kati yao, nami nimewatia mkononi mwa Shetani,^b ili wafundishwe kwa nidhamu wasikufuru.

2 Basi, kwanza kabisa, ninahimiza kwamba dua, shukrani, sala, na maombi yatolewe kwa ajili ya watu wa namna zote, **2** kutia ndani wafalme na wote wenye vyeo vya juu,^{*c} ili tuendelee kuisihi kwa amani na utulivu na ujitoaji-kimungu^d kamili na kuchukua mambo kwa uzito.^d

3 Jambo hilo ni zuri na linampendeza Mwokozi wetu, Mungu,^e **4** ambaye mapenzi yake ni kwamba watu wa namna zote waokolewe^f na kupata ujuzi sahihi wa kweli. **5** Kwa maana kuna Mungu mmoja,^g na mpatanishi mmoja^h kati ya Mungu na wanaadamu,ⁱ mwanadamu, Kristo Yesu,^j **6** aliyejitoa kuwa fidia inayolingana kwa ajili ya wote^{*k}—hilo litatolewa ushahidi kwa wakati wake unaofaa. **7** Kwa ajili ya ushahidi huo^l niliwekwa rasmi niwe mhubiri na mtume^m—ninasema ukweli, sisemi uwongo—mwalimu wa mataifaⁿ kuhusu imani na kweli.

8 Basi ninatamani kwamba kila mahali wanaume waendeleo kusali, wakiinua mikono yenye ushikamanifu,^o bila hasira^p wala mabishano.^q **9** Vivyo hivyo, wanawake wanapaswa kujipamba kwa mavazi yanayofaa,^{*} kwa kiasi na utimamu wa akili,^r si kwa mitindo ya kusuka nywele,

2:2 *Au "wenye mamlaka." #Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:6 *Au "watu wa namna zote." 2:9 *Au "yenye kuheshimika." #Au "kufanya maamuzi mazuri; busara."

dhababu, lulu, au mavazi ya bei ghali sana,^a **10** bali kwa njia inayowafaa wanawake wanaokiri kwamba wanamutumikia Mungu,^b yaani, kupitia matendo mema.

11 Mwanamke na ajifunze akiwa kimya* na kwa ujiitiisho kamili.^c **12** Simruhusu mwanamke afundishe wala kuwa na mamlaka juu ya mwanamume, bali akae kimya.*^d

13 Kwa maana Adamu aliumbwa kwanza, kisha Hawa.^e

14 Pia, Adamu hakudanganywa, bali mwanamke alidangananywa kabisa^f akawa mtenda dhambi. **15** Hata hivyo, atalindwa kupitia kuzaa watoto,^g maadamu anaendelea* kuwa na imani, upendo, utakatifu, na utimamu wa akili.^h

3 Maneno haya ni yenye kutegegemea: Ikiwa mwanamume anajitahidi kuwa mwanagalizi,ⁱ anatamani kazi nje.

2 Mwanagalizi anapaswa kuwa mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi katika mazoea, mwenye utimamu wa akili,^j mwenye utaratibu, mkaribishaji wageni,^k mwenye uwezo wa kufundisha,^l **3** si mlevi,^m si mkatili,* bali mwenye usawaziko,ⁿ si mgomvi,^o si mtu anayependa pesa,^p **4** mwanamume anayeisimamia* nyumba yake vizuri, mwenye watoto wanaojitiisha na kuchukua mambo kwa uzito^q

5 (kwa maana ikiwa mtu haijui jinsi ya kuisimamia* nyu-

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

2:11 *Au "kwa utulivu." 2:12 *Au "awe mtulivu." 2:15 *Tnn., "wanaendelea." *Au "kufanya maamuzi mazuri; busara." 3:2 *Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." *Au "mkarimu." 3:3 *Au "mtu anayepiga watu." 3:4 *Au "anayeongoza." 3:5 *Au "kuongoza."

SURA YA 2

a 1Pe 3:3, 4

b Met 31:30

c Efe 5:24

d 1Ko 14:34

e Mwa 2:18, 22
1Ko 11:8

f Mwa 3:6, 13

g 1Ti 5:14

h 1Ti 2:9, 10

SURA YA 3

i Mdo 20:28

Tit 1:5-9

j Ro 12:3
1Pe 4:7k Mdo 28:7
1Pe 4:9l 1Ti 5:17
2Ti 2:24
Tit 1:7, 9

m Ro 13:13

n Flp 4:5
Yak 3:17o Ro 12:18
Yak 3:18p Ebr 13:5
1Pe 5:2

q Efe 6:4

Safu ya 2

a 1Ti 5:22

b Mdo 22:12
1Th 4:11, 12c Mdo 6:3
Tit 1:7
1Pe 5:2d 1Ti 1:5
1Ti 1:18, 19
2Ti 1:3
1Pe 3:16

e 1Pe 2:12

f 1Ti 5:13

g Tit 2:3-5

h Ebr 3:6

mba yake mwenyewe, atalitunzaje kutaniko la Mungu?), **6** si mtu aliyegeuka hivi kari-buni,^a ili asiye akawa na kiburi na kuanguka katika hukumu aliyohukumiwa Ibilisi. **7** Pia, anapaswa kushuhudiwa vema na* watu walio nje^b ili asianguke katika shutuma[#] na mtego wa Ibilisi.

8 Vilevile watumishi wa huduma wanapaswa kuchukua mambo kwa uzito, si wenye ndimi mbili,* si wenye kunywa divai nyingi, si wenye pupa ya mapato yasiyo ya haki,^c **9** wakiishika siri takatifu ya imani kwa dhamiri safi.^d

10 Pia, wanapaswa kwanza kujaribiwa* kama wanafaa; ndipo watumike wakiwa wahudumu, kwa kuwa hawana shtaka.^e

11 Vilevile wanawake wanapaswa kuchukua mambo kwa uzito, wasiwe wachongezi,^f wawe wenye kiasi katika mazoea, na waaminifu katika mambo yote.^g

12 Watumishi wa huduma wanapaswa kuwa waume wa mke mmoja, wanaosimamia vizuri watoto wao na nyumba zao wenyewe. **13** Kwa maana wanaume wanaohudumu vizuri wanajipatia sifa nzuri na uhuru mwingi wa kusema katika imani iliyo katika Kristo Yesu.

14 Ninakuandikia mambo haya, ingawa ninatumaini kuja kwako upesi, **15** ili nikichelewa ujue jinsi unavyopaswa kutenda katika nyumba ya Mungu,^h ambayo ni kutaniko la Mungu aliyehai,

3:7 *Au "kuwa na sifa nzuri kutoka kwa" *Au "asipate aibu." 3:8 *Au "waseme kwa unyoofu." 3:10 *Au "wajaribiwe kama wanastahili."

nguzo na tegemezo la ile kweli. **16** Kwa kweli, siri takatifu ya huu ujitoaji-kimungu* ni kubwa: 'Alifunuliwa katika mwili,^a alitangazwa kuwa mwadilifu katika roho,^b aliwatokea malaika,^c alihubiriwa kati ya mataifa,^d watu walimwamini ulimwenguni,^e akapokewa mbinguni kwa utukufu.'

4 Hata hivyo, neno lililoo-ngozwa na roho linasema* wazi kwamba wakati ujabo watu fulani wataiacha imani, wakiskiliza maneno ya uwongo yaliyoongozwa na roho waovu^{#f} na mafundisho ya roho waovu, **2** kupitia unafiki wa watu wanaosema uwongo,^g ambao dhamiri zao zimetiwa alama kama kwa chuma cha moto. **3** Wanakataza watu kufunga ndoa^h na kuwaamuru wasile vyakulaⁱ ambavyo Mungu aliumba viliwe^j kwa shukrani na watu wenyewe imani^k na wanaojua kweli kwa usahihi. **4** Kwa sababu kila kiumbe cha Mungu ni kizuri,^l na hakuna kitu kinachopaswa kukataliwa^m ikiwa kinapokewa kwa shukrani, **5** kwa maana kinatakaswa kupitia neno la Mungu na kutolewa sala.

6 Ukiwapa akina ndugu mashauryi haya utakuwa mhadumu mzuri wa Kristo Yesu, aliyelisha maneno ya imani na fundisho bora ambalo umefuata kwa makini.ⁿ **7** Lakini kataa hadithi za uwongo zisizo na heshima,^o kama zile zinazosimuliwa na wanawake wazee. Badala yake, endelea kujizoeza ukiwa na lengo

3:16; 4:7, 8 * Angalia Kamusi, uku. 2012. 4:1 *Tnn., "roho inasema." *Tnn., "roho wadanganyifu."

SURA YA 3

a Yoh 1:14

Flp 2:7

b 1Pe 3:18

c 1Pe 3:19, 20

d Kol 1:23

e Kol 1:6

SURA YA 4

f 2Th 2:1, 2

2Ti 4:3, 4

2Pe 2:1

g Mdo 20:29, 30

2Ti 2:16

2Pe 2:3

h 1Ko 7:36

1Ko 9:5

i Ro 14:3

j Mwa 9:3

k Ro 14:17

1Ko 10:25

l Mwa 1:31

m Mdo 10:15

n 2Ti 2:15

o 1Ti 6:20

Tit 1:13, 14

Safu ya 2

a Yoh 17:3

b Lu 13:24

c Yud 25

d 1Ti 2:3, 4

e Kol 4:16

1Th 5:27

f Mdo 6:5, 6

Mdo 13:2, 3

Mdo 19:6

2Ti 1:6

g 2Ti 4:2

h 1Ko 9:22

SURA YA 5

i Law 19:32

la ujitoaji-kimungu.* **8** Kwa maana mazoezi ya kimwili ni yenye faida kidogo, lakini ujitoaji-kimungu* una faida katika mambo yote, kwa kuwa una ahadi ya uhai wa sasa na ule utakaokuja.^a **9** Maneno hayo ni yenye kutegemeka na yanastahili kukubaliwa kabisa. **10** Hiyo ndiyo sababu tunafanya kazi kwa bidii na kujitahidi,^b kwa sababu tumemtumaini Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi^c wa watu wa namna zote,^d hasa wa walio waaminifu.

11 Endelea kutoa amri hizi na kuzifundisha. **12** Usiruhusu kamwe mtu yeyote audharau ujana wako. Badala yake, uwe mfano mzuri kwa waaminifu katika kusema, katika mwenendo, katika upeendo, katika imani, na katika usafi wa kiadili. **13** Mpaaka nitakapokuja, endelea kujitahidi kusoma mbele ya watu,^e kuhimiza,* na kufundisha. **14** Usipuuze zawadi uliyo nayo uliyopokea kupitia unabii, baraza la wazee lilipoweka mikono juu yako.^f

15 Tafakari* mambo haya; zama katika hayo, ili maendeleo yako yaonekane wazi kwa watu wote. **16** Jianganalie daima wewe mwenyewe na kufundisha kwako.^g Endelea kufanya mambo haya, kwa maana ukifanya hivyo utajiokoa wewe mwenyewe na wale wanaokusikiliza pia.^h

5 Usimkosoe kwa ukali mwanamume mzee.ⁱ Badala yake, msihi kama baba, wanaume vijana kama ndugu, **2** wanawake wazee kama mama, na wanawake vijana

4:13 *Au "kutia moyo." 4:15 *Au "Fikiria kwa makini."

kama dada, kwa usafi wote wa kiadili.

3 Wajali* wajane ambao ni wajane kwelikweli.^{#a} **4** Lakini ikiwa mjane yeyote ana watoto au wajukuu, wanapaswa kwanza kujifunza ujitoajikimungu* katika nyumba zao wenyewe^b na kuwalipa wazazi wao na wazazi wa wazazi wao kinachowastahili,^c kwa maana hilo linakubalika machoni pa Mungu.^d **5** Basi mwanamke ambaye ni mjane kwelikweli na aliye maskini anamtumaini Mungu^e naye huendelea kusali na kutoa dua usiku na mchana.^f **6** Lakini mwanamke anayefuatilia tamaa za mwili amekufa ingawa yuko hai. **7** Basi endelea kuwapa maagizo haya,* ili wasiwe na lawama. **8** Hakika ikiwa yeyote hawaandalii mahitaji watu wake mwenyewe, hasa watu wa nyumba yake, amekana imani naye ni mbaya kuliko mtu asiye na imani.^g

9 Mweke kwenye orodha mjane mwenye umri usiopungua miaka 60, ikiwa alikuwa mke wa mume mmoja, **10** alijulikana kwa kutenda mema,^h alilea watoto,ⁱ alikuwa akiwakaribisha wageni,^{*j} aliiosha miguu ya watakatifu,^k aliwasaidia watu wenye taabu,^l na akajitolea kufanya kila kazi njema.

11 Kwa upande mwingine, usiwaweke kwenye orodha wajane wenye umri mdogo, kwa maana tamaa zao za ngono zinapokuja kati yao na Kristo, wao hutamani

5:3 *Tnn., "Waheshimu." 5:3, 16 *Au "wajane maskini"; yaani, wasio na mtu wa kuwasaidia. 5:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 5:7 *Au "amri hizi." 5:10 *Au "alikuwa mkarimu."

SURA YA 5

a 1Ti 5:16

b 1Ti 5:8

c Mt 15:4
Efe 6:2

d Yak 1:27

e 1Ko 7:34

f Lu 2:36, 37

g Mt 15:4-6

h Mdo 9:39

i 1Ti 2:15

j Ebr 13:2
1Pe 4:9

k Yoh 13:5, 14

l 1Ti 5:16
Yak 1:27

Safu ya 2

a 2Th 3:11

b 1Ko 7:8, 9

c 1Ti 2:15

d Kum 15:11
1Ti 5:5
Yak 1:27

e 1Pe 5:2, 3

f Mdo 28:10
Ebr 13:17g 1Th 5:12
Ebr 13:7h Kum 25:4
1Ko 9:7, 9i Law 19:13
Mt 10:9, 10
Lu 10:7
Gal 6:6j Kum 19:15
Mt 18:16k Tit 1:7, 9
Tit 1:13
Ufu 3:19l 1Ko 15:34
1Yo 3:9

kuolewa. **12** Nao watahukumiwa kwa sababu wameacha imani waliyoonyesha mwanzoni.* **13** Vilevile wanakuwa na tabia ya kupoteza muda, wakizunguka kutoa nyumba moja hadi nyingine; ndiyo, hawapotezi muda tu, bali pia wanapiga porojo na kujiingiza katika mambo ya watu wengine,^a wakiongea kuhusu mambo ambayo hawapaswi. **14** Kwa hiyo, ninatamani wanawake wajane walio na umri mdogo waolewe,^b wazae watoto,^c wasimamie nyumba, ili wasimpe mpinzani sababu ya kukosoa. **15** Kwa kweli, tayari baadhi yao wamepotoshwa na kumfuata Shetani. **16** Ikiwa mwanamke yeyote mwamini ana watu wa ukoo ambao ni wazae, inafaa awasaidie ili kutaniko lisibebe mzigo huo, na hivyo liwasaidie wale walio wajane kwelikweli.^{#d}

17 Wazee wanaosimamia kwa njia nzuri^e wanastahili heshima mara mbili,^f hasa wale wanaofanya kazi kwa bidii katika kusema na kufundisha.^g **18** Kwa maana andiko linasema, "Hupaswi kumfunga kinywa ng'ombe dume anapopura nafaka,"^h pia, "Mfanyakazi anastahili mshahara wake."ⁱ **19** Usikubali mashtaka dhidi ya mwanamume mzee,* isipokuwa kwa ushahidi wa mashahidi wawili au watatu.^j **20** Wakaripie^k hadharani watu wanaozoea kutenda dhambi,^l ili liwe onyo kwa wengine.* **21** Ninakuagiza kwa uzito mbele za Mungu na Kristo Yesu na

5:12 *Au "ahadi waliyotoa mwanzoni." 5:19 *Au "mzee." 5:20 *Tnn., "ili wengine waogope."

malaika waliochaguliwa, ufuate maagizo haya bila kubagua wala kupendelea.^a

22 Usiharakishe kamwe kuweka mikono yako juu ya* mwanamume yeyote;^b wala usishiriki dhambi za wengine; endelea kuwa safi.

23 Usiendeleo kunywa maji,* bali unywe divai kidogo kwa ajili ya tumbo lako na ugonjwa wako wa mara kwa mara.

24 Dhambi za watu fulani hujulikana hadharani, na hivyo wanahukumikiwa moja kwa moja, lakini dhambi za watu wengine hujulikana baadaye.^c **25** Vivyo hivyo, mate ndo mema hujulikana hadharani^d na hata yale yasiyojulikana hayawezi kuendelea kufichwa.^e

6 Acheni wale walio chini ya nira ya utumwa waendeleo kuwaheshimu kikamili^f mabwana wao, ili watu wasiseme vibaya kuhusu jina la Mungu na lile fundisho.^g **2** Pia, acheni wale walio na mabwana ambao ni waamini wasi wavunjie heshima kwa sababu wao ni ndugu zao. Badala yake, wanapaswa kuwatumikia kwa bidii zaidi, kwa sababu wale wanaonufaika na utumishi wao mzuri ni waamini wenzao wapendwa.

Endelea kuwafundisha na kuwahimiza wafanye mambo haya. **3** Mtu yeyote akifundisha mafundisho tofauti na yanayopingana na fundisho lenye manufaa*^h linalotoka kwa Bwana wetu Yesu Kristo, au mafundisho yasiyopatana na ujitoaji-kimungu,ⁱ **4** yeye

5:22 *Yaani, usimweke rasmi mtu yeyote haraka haraka. 5:23 *Au "Usinywe maji tu." 6:3 *Au "lenye afya; lenye faida." 6:3, 5, 6, 11 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 5

a Law 19:15
Yak 3:17

b Mdo 6:5, 6
Mdo 14:23
1Ti 3:2, 6
1Ti 4:14

c Yos 7:11
Ebr 4:13

d Mt 5:16

e 1Ko 4:5

SURA YA 6

f Ro 13:7
Efe 6:5
Kol 3:22

g 1Pe 2:13, 14

h 2Ti 1:13

i Tit 1:1, 2

Safu ya 2

a 1Ko 8:2

b 2Ti 2:14
Tit 1:10
Tit 3:9

c 2Ko 11:3
2Ti 3:8
Yud 10

d 1Pe 5:2

e 1Ti 4:8

f Ayu 1:21
Zb 49:16, 17

g Met 30:8, 9
Ebr 13:5

h Mt 13:22

i Met 28:20, 22
Yak 5:1

j Mt 6:24

k Met 15:1
Mt 5:5
Gal 5:22, 23
Kol 3:12
1Pe 3:15

anajivuna kwa kiburi na haelewi chochote.^a Pia, anapenda sana* kubishana na kushindana kuhusu maneno.^b Mambo hayo huleta wivu, mizozo, uchongezi,[#] na shaka zenye uovu, 5 mabishano ya kawaida kuhusu mambo madogo madogo ya watu waliopotoka kiakili^c na wasiojua kweli, wakifikiri ujitoaji-kimungu[#] ni njia ya kupata faida.^d **6** Kwa hakika, kuna faida kubwa ya kuwa na ujitoaji-kimungu^{#e} na kuridhika.* **7** Kwa maana hatukuleta chochote ulimwenguni, wala hatuwezi kuondoka na chochote.^f **8** Basi, tu kiwa na chakula* na mavazi,[#] tutaridhika na vitu hivyo.^g

9 Lakini wale ambao wameazimia kuwa matajiri huanuka kwenye majaribu, na mtego,^h na tamaa nyingi za kijinga zenye kudhuru ambazo hutumbukiza watu kwenye maangamizi na uharibifu.ⁱ **10** Kwa maana kupenda pesa ndicho chanzo cha mambo mbaya ya kila aina, na kwa kujitahidi kufikia upendo huo, wengine wamepotoshwa kutoka kwenye imani na kujichoma kila mahali kwa mauivu mengi.^j

11 Ingawa hivyo, wewe, mtu wa Mungu, yakimbie mambo hayo. Badala yake, fuatilia uadilifu, ujitoaji-kimungu,[#] imani, upendo, uvumilivu, na upole.^k **12** Pigana pigano zuri la imani, ushike imara uzima wa milele ulioitiwa nawe ukatoa tangazo zuri la hadharani mbele ya mashahidi wengi.

6:4 *Au "anapenda isivyo kawaida." #Au "matusi." 6:6 *Tnn., "pamoja na ujitoshelivu." 6:8 *Au "riziki." #Au labda, "makao." Tnn., "kitu cha kujifunika."

13 Mbele za Mungu, anayevihifadhi vitu vyote hai, na Kristo Yesu, ambaye akiwa shahidi alitoa tangazo zuri la hadharani mbele ya Pontio Pilato,^a ninakuagiza 14 uishi-ke amri katika njia safi na isiyolaumika mpaka wakati wa ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo,^b 15 ambao yule Mtwala Mkuu wa pekee na mwenye furaha atauonyesha katika nyakati zake zilizowekwa. Yeye ndiye Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana,^c 16 yeye peke yake asiye-yeza kufa,^d anayeishi katika nuru isiyoweza kufikiwa^e na ambaye hakuna mwanadamu amemwona wala anayeweza kumwona.^f Kwake na kuwe na heshima na nguvu milele. Amina.

17 Waagize* wale walio matajiri katika mfumo wa

6:17 *Au "Waamuru."

SURA YA 6

- a Mt 27:11
Yoh 18:33, 36
Yoh 19:10, 11
- b 2Th 2:8
2Ti 4:1, 8
- c Ufu 17:14
Ufu 19:16
- d Ebr 7:15, 16
- e Mdo 9:3
Ufu 1:13, 16
- f Yoh 14:19
1Pe 3:18

Safu ya 2

- a Mt 13:22
Mk 10:23
- b Mhu 5:19
Mt 6:33
Yak 1:17
- c Ro 12:13
2Ko 8:14
Yak 1:27
- d Mt 6:20
- e Lu 16:9
- f 2Ti 1:13, 14
2Ti 3:14
2Ti 4:5
- g 1Ko 2:13
1Ko 3:19
Kol 2:8

mambo* wa sasa wasijivune[#] wala wasiutumaini utajiri usiotegemeka,^a bali wamtumaini Mungu, ambaye hutupatia kwa wingi vitu vyote tunavyofurahia.^b 18 Waambie watende mema, wawe matajiri katika matendo mazuri, wawe wakarimu, tayari kushiriki vitu na wengine,^c 19 wakijiweka salama hazina ya msingi mzuri kwa ajili ya wakati ujao,^d ili waushike imara uzima ulio wa kweli.^e

20 Timotheo, linda yote uliyokabidhiwa,^f jiepuche na maneno matupu yanayochafua mambo matakatifu na pia uepuke mawazo yanayopingana ya "ujuzi" wa uwongo.^g

21 Kwa kujisifia ujuzi huo, wengine wameiacha imani.

Fadhili zisizostahiliwa na ziwe pamoja nawe.

6:17 *Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "wasijitakie makuu."

BARUA YA PILI KWA

TIMOTHEO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1, 2)
Paulo amshukuru Mungu kwa sababu ya imani ya Timotheo (3-5)
Endelea kuchochea kama moto zawadi ya Mungu (6-11)
Endelea kushika maneno yenye manufaa (12-14)
Maadui na marafiki wa Paulo (15-18)
- 2 Wakabidhi ujumbe wanaume wanaostahili (1-7)
Kuvumilia mateso kwa ajili ya habari njema (8-13)

- Litumie sawasawa neno la Mungu (14-19)
Zikimbie tamaa za ujana (20-22)
Jinsi ya kushughulika na wapinzani (23-26)
- 3 Nyakati hatari katika siku za mwisho (1-7)
Fuata mfano wa Paulo kwa ukaribu (8-13)
"Endelea kufuata mambo uliyojifunza" (14-17)
Kila Andiko limeongozwa na roho ya Mungu (16)

- 4 “Timiza kikamili huduma yako” (1-5)
 Hubiri neno kwa uharaka (2)
 “Nimepigana pigano zuri” (6-8)
 Maelezo ya binafsi (9-18)
 Salamu za mwisho (19-22)

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu kulingana na ahadi ya uzima ambao ni kupitia Kristo Yesu,^a **2** kwa Timotheo, mto-
 mo mpendwa:^b

Na uwe na fadhili zisizostahiliwa, rehema, na amani kutoka kwa Mungu Baba na Kristo Yesu Bwana wetu.

3 Ninamshukuru Mungu, ninayemtotea utumishi mtakatifu kama mababu zangu walivyofanya, na nikiwa na dhambi safi, siachi kamwe kukumbuka katika dua zangu usiku na mchana. **4** Ninapokumbuka machozi yako, ninatamani kukuona ili nijawe na shangwe. **5** Kwa maana ninaikumbuka imani yako isiyona na unafiki,^c ambayo kwanza ilikuwa ndani ya nyanya yako Loisi na mama yako Eunike, lakini ambayo nina hakika imo ndani yako pia.

6 Kwa sababu hii ninakukumbusha uichochee kama moto zawadi ya Mungu iliyo ndani yako uliyopokea nilipoweke mikono yangu juu yako.^d **7** Kwa maana Mungu hakutupatia roho ya woga,^e bali roho ya nguvu^f na ya upendo na ya utimamu wa akili. **8** Basi usione aibu kuhusu ushahidi juu ya Bwana wetu,^g au kunihusu mimi, mfungwa kwa ajili yake, bali shiriki katika kuvumilia dhiki^h kwa ajili ya habari nje-

SURA YA 1

- a Yoh 3:16
 Yoh 6:40, 44
 1Pe 1:3, 4
 b 1Ko 4:17
 c 1Ti 4:6
 d 1Ti 4:14
 e Ro 8:15
 1Th 2:2
 f Lu 24:49
 Mdo 1:8
 g Ro 1:16
 h Kol 1:24
 2Ti 2:3

Safu ya 2

- a Flp 4:13
 Kol 1:11
 b Efe 1:4
 Ebr 3:1
 c Efe 2:5
 Efe 2:8
 Tit 3:5
 d Yoh 1:14
 Ebr 2:9
 e 1Ko 15:54
 Ebr 2:14
 f Yoh 5:24
 1Yo 1:2
 g 1Pe 1:3, 4
 h Ro 1:16
 i Mdo 9:15
 1Ti 2:7
 j Mdo 9:16
 Efe 3:1
 k 2Ko 4:2
 l 2Ti 4:8
 m 1Ti 6:3, 4
 Tit 1:7, 9
 n Ro 8:11

ma kwa kutegemea nguvu za Mungu.^a **9** Yeye alituokoa na kutuita kwa mwito mtakatifu,^b si kwa sababu ya mate-
 ndo yetu, bali kwa sababu ya kusudi lake mwenyewe na fadhili zisizostahiliwa.^c Tuli-
 pewa fadhili hizo kuhusiana na Kristo Yesu kabla ya nyakati za kale, **10** lakini sasa zimefanywa kuwa wazi kabisa kupitia ufunuo wa Mwokozi wetu, Kristo Yesu,^d ambaye amefuta kifo^e na kuangaza nuru juu ya uzima^f na kutoweza kuharibika^g kupitia habari njema,^h **11** ambayo kwa ajili yake mimi niliwekwa rasmi kuwa mhubiri na mtume na mwalimu.ⁱ

12 Ndiyo sababu ninavumilia pia mambo haya,^j lakini sioni aibu.^k Kwa maana ninamjua Yule ambaye nimemwamini, nami nina uhakika kwamba anaweza kulinda kile nilichoweka amana kwake mpaka siku hiyo.^l **13** Endelea kushika kigezo cha* maneno yenye manufaa^m uliyosikia kutoka kwangu kwa imani na upendo unaotokana na muungano pamoja na Kristo Yesu. **14** Linda amana hii nzuri kupitia roho katatifu, inayokaa ndani yetu.ⁿ

15 Unajua jambo hili, kwamba watu wote katika mkoa

1:13 *Au “kielelezo cha.” #Au “yenye afya; yenye faida.”

wa Asia^a wameniacha, Figelolo na Hermogene ni kati yao. **16** Bwana na aionyeshe rehema nyumba ya Onesiforo,^b kwa maana aliniburudisha mara nyingi, naye hakuabika kwa sababu ya minyororo yangu ya gereza. **17** Kinyume chake, alipokuwa Roma, alinitafuta kwa bidii mpaka akani-pata. **18** Bwana na amruhusu apate rehema kutoka kwa Yehova* katika siku ile. Nawe unajua vema utumishi wote aliofanya huko Efeso.

2 Kwa hiyo, wewe mwana-ngu,^c endelea kujipatia nguvu katika fadhili zisizo-stahiliwa zilizo katika Kristo Yesu; **2** na mambo uliyoyasikia kutoka kwangu yaliyothibitishwa na mashahidi wengi,^d mambo hayo uwakabidhi wanaume waaminifu, ambao watastahili vya kutosha kuwafundisha wengine. **3** Ukiwa mwanajeshi mwema^e wa Kristo Yesu, shiriki katika kuvumilia dhiki.^f **4** Mtu anayetumikia akiwa mwanajeshi hajihusishi* katika shughuli za kibiashara[#] za maisha, ili apate kibali cha yule aliyemwandikisha kuwa mwanajeshi. **5** Hata katika michezo, yeyote anayeshindana havikwi taji asiposhindana kulingana na sheria.^g **6** Mkulima anayefanya kazi kwa bidii lazima awe wa kwanza kula matunda. **7** Fikiria daima mambo ninayosema; Bwana atakupatia uelewaji* katika mambo yote. **8** Kumbuka kwamba Yesu Kristo alifufuliwa kutoka kwa wafu^h na alikuwa uzao

1:18 *Angalia Nyongeza A5. 2:4 *Tnn., "hajifungi." #Au labda, "shughuli za kila siku." 2:7 *Au "utambuzi."

SURA YA 1

a Mdo 19:10

b 2Ti 4:19

SURA YA 2

c 1Ti 1:2

d 2Ti 3:14

e 1Ti 1:18

f 2Ti 1:8

g 1Ko 9:25

h Mdo 2:24

Safu ya 2

a Mdo 2:29-32
Ro 1:3

b Mdo 13:23

c Mdo 9:16
Flp 1:7

d Kol 4:3, 4

e 2Ko 1:6
Efe 3:13
Kol 1:24

f Ro 6:5, 8

g Ufu 3:21
Ufu 20:4, 6h Mt 10:33
Lu 12:9

i 2Ti 4:2

j 1Ti 4:7
1Ti 6:20

k 1Ti 1:20

l 1Ko 15:12

wa Daudi,^{*a} kulingana na habari njema ninayohubiri,^b **9** ambayo kwa ajili yake ninavumilia na kufungwa gereza ni kama mhalifu.^c Hata hivyo, neno la Mungu halifungwi.^d **10** Kwa sababu hiyo ninaendelea kuvumilia mambo yote kwa ajili ya wale waliochaguliwa,^e ili wao pia wapate wokovu ambao ni kupitia Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele. **11** Maneno haya yanategemeka: Hakika ikiwa tulikufa pamoja, tutaishi pamoja pia;^f **12** tukiendelea kuvumilia, tutatawala pamoja pia tukiwa wafalme;^g tukimkana, naye pia atatukana sisi;^h **13** tukikosa kuwa waaminifu, yeye anabaki kuwa mwaminifu, kwa maana hawezi kujikana mwenyewe.

14 Endelea kuwakumbusha mambo haya, ukiwaagiza* mbele za Mungu wasipigane kuhusu maneno, jambo hilo halina faida kabisa kwa sababu linawadhuru[#] wale wanaosikiliza. **15** Fanya yote unayoweza ili ujitoe kwa Mungu ukiwa mtu aliyekubaliwa, mfanakazi asiye na lolote la kuonea aibu, ukilitumia sawasawa neno la kweli.ⁱ **16** Lakini kataa maneno matupu ambayo huchafua mambo matakatifu,^j kwa maana yataongoza kwenye kutomwogopa Mungu zaidi na zaidi, **17** na neno lao litaenea kama kidonda kinachooza. Himenayo na Fileto ni kati yao.^k **18** Watu hao wamegeuka kutoka kwenye kweli, wakisema kwamba tayari ufufua umetukia,^l nao wanapindua imani ya wengi-

2:8 *Tnn., "wa mbegu ya Daudi." 2:14 *Tnn., "ukiwatolea ushahidi kamili." #Au "linawaharibu; linawavuruga."

ne. **19** Ingawa hivyo, msingi imara wa Mungu unakaa ukiwa umesimama, ukiwa na muhuri huu: "Yehova* anawajua walio wake,"^a na "Kila mtu anayeliitia jina la Yehova*^b na aukatae ukosefu wa uadilifu."

20 Basi ndani ya nyumba kubwa kuna vyombo vya dhababu na fedha, na pia kuna vyombo vya miti na vya udongo, na vingine ni vya matumizi yanayoheshimika lakini vingine ni vya matumizi yasiyoheshimika. **21** Kwa hiyo, yeyote akijiepusha na hivyo vya mwisho, atakuwa kifaa* cha matumizi yanayoheshimika, kilichotakaswa, chenye faida kwa bwana wake, kilichotayarishwa kwa ajili ya kila kazi njema. **22** Basi zikimbie tamaa za ujana, lakini fuatilia uadilifu, imani, upendo, amani, pamoja na wale wanaomwitia Bwana kwa moyo safi.

23 Isitoshe, kataa mabishano ya kipumbavu na ya kijianga,^c ukijua kwamba hayo hutokeza mapigano. **24** Kwa maana mtumwa wa Bwana ha hitaji kupigana, bali anahitaji kuwa mpole* kwa wote,^d mwenye uwezo wa kufundisha, anayejizuia anapokosewa,^e **25** akiwafundisha kwa upole wale wasio na mwelekeo unaofaa.^f Huenda Mungu akawasaidia kutubu* na kupata ujuzi sahihi wa kweli,^g **26** nao warudiwe na fahamu na kutoka kwenye mtego wa Ibilisi, kwa kuwa amewanasa wakiwa hai ili wafanye mapeenzi yake.^h

2:19 *Angalia Nyongeza A5. 2:21 *Au "chombo." 2:24 *Au "mwenye busara." 2:25 *Au "kubadili mawazo."

SURA YA 2

a Hes 16:5

b Isa 26:13

c 1Ti 1:3, 4
1Ti 4:7
Tit 3:9

d 1Th 2:7

e Mt 5:39

f Met 15:1
Gal 6:1
Tit 3:2
1Pe 3:15

g 1Ti 2:3, 4

h Yoh 13:27
Mdo 5:3
1Ti 1:20

Safu ya 2

SURA YA 3

a Mt 24:3
1Ti 4:1
2Pe 3:3
Yud 17, 18b Mt 7:15
Mt 7:22, 23c Kut 7:11, 12
Kut 9:11d 1Ko 4:17
2Ti 1:13

3 Lakini ujue jambo hili, kwamba katika siku za mwisho^a kutakuwa na nyakati za hatari zilizo ngumu kushughulika nazo. **2** Kwa maana watu watakuwa wenye kujienda wenyewe, wenye kupeenda pesa, wenye kujidai, wenyewe majivuno, wakufuru, wasiotii wazazi, wasio na shukrani, wasio washikamanifu, **3** wasio na upendo wa asili, wasiotaka makubaliano yoyote, wachongezi, wasiojizua,* wakali, wasiopenda wema, **4** wasaliti, wenye vichwa vigumu, waliojaa kiburi, wanaopenda raha badala ya kumpeenda Mungu, **5** wakionekana kama watu wanaomwogopa Mungu lakini wakizikana nguvu zake;^b nawe jiepuse nao. **6** Kutoka miongoni mwao hini nuka watu wanaoingia kwa ujanja katika nyumba na kuwachukua mateka wanawake walio dhaifu ambao wamelemewa na mizigo ya dhambi, wakiongozwa na tamaa mbalimbali, **7** wakijifunza sikuzote lakini hawawezi kamwe kupata ujuzi sahihi wa kweli.

8 Basi kama vile Yane na Yambre walivyompinga Musa, vivyo hivyo hawa pia wanaendelea kuipinga kweli. Watu hao wamepotoshwa akili kabisa, wakiwa wamekataliwa kuhusiana na imani. **9** Hata hivyo, hawatafanya maendeleo zaidi, kwa maana upumbavu* wao utakuwa wazi kwa watu wote, kama ilivyo kuwa kwa watu hao wawili.^c **10** Lakini wewe umefuata kwa ukaribu fundisho langu, mwendo wangu wa maisha,^d

3:3 *Au "wasiojidhibiti." 3:9 *Au "ujinga."

kusudi langu, imani yangu, subira yangu, upendo wangu, uvumilivu wangu, **11** mate-so na shida kama zile nilizopata huko Antiokia,^a Ikoniamu,^b na Listra.^c Nilivumilia mate-so hayo, naye Bwana alinioko kutoka katika hayo yote.^d **12** Kwa kweli, wote wanaotamani kuishi kwa ujitoajikimungu* katika ushirika na Kristo Yesu watateswa pia.^e **13** Lakini watu waovu na wajanja wataendelea kutoka ubaya mpaka ubaya zaidi, waki-potosha na kupotosha.^f

14 Hata hivyo, endelea ku-fuata mambo uliyojifunza na uliyoshawishiwa kuamini,^g ukijua ulijifunza mambo hayo kutoka kwa nani, **15** na kwa-amba tangu utoto mchanga^h umeyajua maandishi mataka-tifu,ⁱ ambayo yanaweza kuku-fanya uwe mwenye hekima ili upate wokovu kupitia imani katika Kristo Yesu.^j **16** Kila Andiko limeongozwa na roho ya Mungu^k nalo ni lenye faida kwa kufundisha,^l kwa kukaripia, kwa kunyoosha* mambo, kwa kutia nidhamu katika uadilifu,^m **17** ili mtu wa Mungu awe na uwezo kamili, akiwa na vifaa kamili kwa ajili ya kila kazi njema.

4 Ninakuagiza kwa uzito mbele za Mungu na Kristo Yesu, ambaye atawahukumuⁿ walio hai na wafu,^o na kwa ufunuo^p wake na Ufalme wake:^q **2** Lihubiri neno;^r fanya hivyo kwa uharaka katika nyakati zinazofaa na nyakati ngumu; karipia,^s kemea, himiza, kwa subira yote na ustadi wa kufundisha.^t **3** Kwa maa-

3:12; 4:10 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 3:16 *Au "kurekebisha."

SURA YA 3

a Mdo 13:50
b Mdo 14:1, 5, 6
c Mdo 14:19
d 2Ko 1:10
e Mt 16:24
Yoh 15:20
Mdo 14:22
f 2Th 2:11
1Ti 4:1
g 2Ti 1:13
h Met 22:6
i Mdo 16:1, 2
j Yoh 5:39
k Yoh 14:26
2Pe 1:21
l Ro 15:4
m 1Ko 10:11

SURA YA 4

n Yoh 5:22
Mdo 17:31
2Ko 5:10
o Yoh 5:28, 29
Mdo 10:42
p 1Ti 6:14, 15
1Pe 5:4
q Ufu 11:15
Ufu 12:10
r 2Ti 2:15
s 1Ti 5:20
Tit 1:7, 9
Tit 1:13
Tit 2:15
t 2Ti 2:24, 25

Safu ya 2

a 1Ti 1:9, 10
b 1Ti 4:1
c 2Ti 1:8
2Ti 2:3
d Ro 15:19
Kol 1:25
e Hes 28:6, 7
f Flp 1:23
g 1Ko 9:26
1Ti 6:12
h Flp 3:14
i 1Ko 9:25
Yak 1:12
j Yoh 5:22
k 1Pe 5:4
Ufu 2:10
l Kol 4:14
Flm 23, 24
m Efe 6:21
Kol 4:7

na kutakuwa na wakati ambapo hawatalivumilia fundisho lenye manufaa,^{*a} bali, kulingana na tamaa zao, watajikusanyia walimu ili masikio yao yafurahishwe.^{#b} **4** Wataacha kuisikiliza ile kweli, nao watageukia hadithi za uwongo. **5** Ingawa hivyo, wewe tunza akili zako katika mambo yote, vumilia hali ngumu,^c fanya kazi ya mweneza-injili,^{*} timiza kikamili huduma yako.^d

6 Kwa maana mimi tayari ninamiminwa kama toleo la kinywaji,^e na wakati wangu wa kufunguliwa^f umekaribia sana. **7** Nimepigana pigano zuri,^g nimekimbia mbio mpaka mwisho,^h nimeishika imani. **8** Tangu sasa na kuendelea nimewekewa akiba ya taji la uadilifu,ⁱ ambalo Bwana, aliye mwamuzi mwadilifu,^j atanipa kuwa thawabu katika siku ile,^k lakini si mimi tu, bali pia wote ambao wamependa kufunuliwa kwake.

9 Jitahidi kabisa ili uje kwangu upesi. **10** Kwa maana Dema^l ameniacha kwa sababu aliupenda mfumo wa mambo* wa sasa, naye ameenda Thesalonike, Kresensi ameenda Galatia, Tito ameenda Dalmatia. **11** Luka tu ndiye aliye pamoja nami. Mchukue Marko uje pamoja naye, kwa maana ni mwenye faida kwangu katika huduma. **12** Lakini nime-tuma Tikiko^m aende Efeso. **13** Utakapokuja, ilete ile kanzu niliyomwachia Karpo kule Troa, na vile vitabu vya kukunjwa, hasa vile vya ngozi.

4:3 *Au "lenye afya; lenye faida." #Au "waambiwe mambo wanayotaka kusikia." 4:5 *Au "endelea kuhubiri habari njema."

14 Aleksanda yule fundi wa shaba alinisababishia madhara mengi. Yehova* atamlipa kulingana na matendo yake.^a

15 Nawe pia jihadhari naye, kwa maana aliupinga ujumbe wetu kwa kadiri kubwa sana.

16 Katika kujitetea kwangu mara ya kwanza hakuna yeyote aliyekuja upande wangu, bali wote waliniacha—wasihukumiwe kwa jambo hilo.

17 Lakini Bwana alisimama karibu nami na kunitia nguvu, ili kupitia kwangu kazi ya kuhubiri itimizwe kikamili na mataifa yote yaisikie;^b nami niliokolewa kutoka katika kinywa cha simba.^c **18** Bwana atanikomboa kutoka ka-

4:14 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 4

a Zb 28:4
Zb 62:12
Met 24:12

b Mdo 9:15

c Zb 22:21

Safu ya 2

a Ufu 20:4

b Ro 16:3

c 2Ti 1:16

d Mdo 19:22

e Mdo 21:29

2 TIMOTHEO 4:14 - TITO 1:3

tika kila tendo la uovu naye ataniokoa kwa ajili ya Ufalme wake wa mbinguni.^a Utukufu na uwe kwake milele na milele. Amina.

19 Uwape salamu zangu Priska na Akila^b na nyumba ya Onesiforo.^c

20 Erasto^d alibaki Korintho, lakini nilimwacha Trofimo^e akiwa mgonjwa huko Mileto. **21** Jitahidi kabisa ili ufike kabla ya majira ya bari-di kali.

Eubulo anakutumia salamu zake, na pia Pudensi na Lino na Klaudia na ndugu wote.

22 Bwana na awe pamoja na roho unayoonyesha. Fadhili zake zisizostahiliwa na ziwe pamoja nawe.

KWA

TITO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1-4)
Tito aagizwa kuweka rasmi wazee huko Krete (5-9)
Wakaripie wale wanaoasi (10-16)
- 2 Ushauri unaofaa kwa wazee na vijana (1-15)
Kataa matendo yasiyompendeza Mungu (12)

- Bidii kwa ajili ya matendo mema (14)
- 3 Kujitiisha kwa njia inayofaa (1-3)
Uwe tayari kufanya matendo mema (4-8)
Epuka mabishano ya kipumbavu na madhehebu (9-11)
Maagizo ya kibinafsi na salamu (12-15)

1 Paulo, mtumwa wa Mungu na mtume wa Yesu Kristo kulingana na imani ya waliochaguliwa wa Mungu, na ujuzi sahihi wa ile kweli ambayo inapatana na ujitoaji-

Safu ya 2

SURA YA 1

a Ro 6:23

b Hes 23:19

kimungu* **2** na inayotegemea tumaini la uzima wa milele^a ambao Mungu, asiyeweza kusema uwongo,^b aliahidi zamani za kale; **3** lakini kwa

1:1 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

wakati wake, alifanya neno lake lijulikane kupitia kazi ya kuhubiri ambayo nilikabidhiwa^a kulingana na amri ya Mwokozi wetu, Mungu; **4** kwa Tito, mwanangu halisi kulingana na imani tunayoshiriki:

Na uwe na fadhili zisizostahiliwa na amani kutoka kwa Mungu Baba na Kristo Yesu Mwokozi wetu.

5 Nilikuacha Krete ili urekebise mambo yaliyokuwa na kasoro* na kuweka rasmi wazee katika jiji moja baada ya lingine, kama nilivyokuagiza: **6** ikiwa kuna mwanamume asiye na shtaka, mume wa mke mmoja, mwenye watoto wanaoamini ambao hawana mashtaka ya kuwa wapotovu* au waasi.^b **7** Mwangalizi ni msimamizi aliyechaguliwa na Mungu, hivyo hapaswi kuwa na shtaka, asiwe mshupavu,^c asiwe mwenye kukasirika upepsi,^d asiwe mlevi, asiwe mkatili,* asiwe na pupa ya mapato yasiyo ya haki, **8** bali awe mkaribishaji wageni,*^e anayependa mema, mwenye utimamu wa akili,^f mwadilifu, mshikamanifu,^g anayejidhibiti,^h **9** anayefuata kikamili neno la uaminifu* katika ustadi wake wa kufundisha,ⁱ ili aweze kutia moyo[#] kwa fundisho lenye manufaa^Δ na pia kuwakaripia^k wale ambao hulipinga.

10 Kwa maana kuna watu wengi waasi, wanaoongea maneno yasiyo na faida, na wadanganyifu, hasa wale wanaoshi-

1:5 *Au "upungufu." 1:6 *Au "watu-kutu." 1:7 *Au "asiwe mpiga watu." 1:8 *Au "mkarimu." #Au "anayefanya maamuzi mazuri; mwenye busara." 1:9 *Au "ujumbe wenye kutegemeka." #Au "kuhimiza." 1:9; 2:1 ΔAu "lenye afya; lenye faida."

SURA YA 1

a Mdo 9:15

b 1Ti 3:2-7

c 2Pe 2:10

d Yak 1:19

e 1Pe 4:9

f Ro 12:3
1Ti 3:2

g 1Ti 2:8

h 2Ti 2:24
Yak 3:13i 1Ti 4:16
1Ti 6:3, 4j 1Ti 1:9, 10
2Ti 1:13k 1Ti 5:20
2Ti 4:2
Tit 1:13
Ufu 3:19

Safu ya 2

a Mdo 15:1

b Ro 14:14

c Mt 15:11

d Mt 7:16-18

SURA YA 2

e 1Ti 4:16
2Ti 1:13

kamana na tohara.^a **11** Lazima watu hao wanyamazishwe, kwa sababu wanaendelea kupotosha imani ya nyumba nzima nzima kwa kufundisha mambo ambayo hawapaswi, wakiwa na nia ya kupata mapato yasiyo ya haki. **12** Mmoja wao, nabii wao wenye-we, alisema: "Wakrete ni wango sikuzote, wanyama hatari wa mwituni, walafi wasiofanya kazi."

13 Ushahidi huu ni wa kweli. Kwa sababu hiyo endelea kuwakaripia kwa ukali ili wawe na imani yenye afya, **14** na wasisikilize hadithi za uwongo za Kiyahudi na amri za watu ambao wanaiacha kweli. **15** Vitu vyote ni safi kwa watu safi;^b lakini kwa watu waliochafuliwa na wasio na imani hakuna chochote kilicho safi, kwa kuwa akili na dhamiri zao zimechafuliwa.^c **16** Wao hutangaza hadharani kwamba wanamjua Mungu, lakini wanamkana kwa mateendo yao,^d kwa sababu ni wenye kuchukiza, wasiotii, na wasiostahili kufanya kazi yoyote njema.

2 Hata hivyo, wewe endelea kusema mambo yanayopata na fundisho lenye manufaa.^{Δe} **2** Wanaume wenye umri mkubwa wanapaswa kuwa wenye kiasi katika mazoea, wanaochukua mambo kwa uzito, wenye utimamu wa akili, wenye imani yenye afya, wenye upendo, na wavumilivu. **3** Vilevile wanawake wenye umri mkubwa wanapaswa kuwa wenye tabia ya kumhofu Mungu, wasiwe wachongezi, wala wasiwe watumwa wa divai nyingi, wawe walimu wa yaliyo mema; **4** ili wawa-

shauri* wanawake vijana wawapende waume zao, wawapende watoto wao, **5** wawe na utimamu wa akili, safi kiadili, wanaofanya kazi nyumbani,* wema, wanaojitiisha kwa waume zao,^a ili neno la Mungu lisitukanwe.

6 Vivyo hivyo, endelea kuwahimiza wanaume vijana wawe na utimamu wa akili,^b **7** ukiwawekea mfano mzuri wa matendo mema katika mambo yote. Fundisha mambo safi* kwa uzito wote,^c **8** ukitumia maneno yenye manufaa* yasiyoweza kulau-miwa,^d ili kuwaaibisha wale wanaopinga, wakiwa hawana jambo lolote baya^e la kusema kutuhusu.^e **9** Watumwa na wajinyenyekeze kwa mabwana wao katika mambo yote,^f wakijitahidi kuwapendeza, wasibishane nao, **10** wasiwe wakiwaibia,^g bali wawe waaminifu kabisa, ili katika mambo yote walipambe fundisho la Mwokozi wetu, Mungu.^h

11 Kwa maana Mungu ameyonesha fadhili zisizostahiliwa kwa kuwaletea wokovu watu wa namna zote.ⁱ **12** Nazo zinatuzoeza kukataa matendo yasiyompendeza Mungu na tamaa za ulimwengu^j na kuishi kwa utimamu wa akili, uadilifu, na ujitoaji-kimungu* katika mfumo huu wa mambo,^{#k} **13** huku tusingojea tumaini lenye furaha^l na kufunuliwa kwenye utukufu kwa Mungu mkuu na kwa Mwokozi wetu,

2:4 *Au "wawakumbushe; wawazoeze."

2:5 *Au "wanaotunza nyumba zao."

2:7 *Au labda, "Fundisha kwa usafi."

2:8 *Au "yenye afya; yenye faida."

*Au "ovu."

2:12 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

*Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo."

SURA YA 2

a 1Ko 14:34, 35

1Pe 3:1, 2

b Ro 12:3

1Pe 5:5

c 2Ti 2:15

d Kol 3:8

e 1Pe 2:15

f Efe 6:5

1Ti 6:1

1Pe 2:18

g Efe 4:28

h Mt 5:16

i Ro 5:18

j 1Yo 2:16

k Ro 12:2

l 1Pe 1:13

Safu ya 2

a Mt 20:28

1Ti 2:5, 6

b Efe 1:7

Kol 1:13, 14

c Efe 2:10

Ebr 9:14

d 2Ti 4:2

SURA YA 3

e Mk 12:17

Ro 13:1

1Pe 2:13, 14

f Flp 4:5

Yak 3:17

g Met 15:1

Gal 6:1

Efe 4:1, 2

1Ti 6:11

2Ti 2:24, 25

1Pe 3:15

h Lu 6:35

Ro 2:4

Efe 4:32

i Kum 9:5

Ro 3:10

Gal 3:21

j Ro 5:15, 21

Ro 6:23

k Ro 5:18

l Yoh 3:5

Ro 8:23

2Ko 5:17

m Mdo 2:33

n Ro 3:24

Gal 2:15, 16

o Ro 8:17

p Ro 6:23

Yesu Kristo, **14** aliyejitoa kwa ajili yetu^a ili atuweke huru^{#b} kutoka katika kila namna ya uasi sheria na kujisafisha watu walio mali yake ya pekee, wenye bidii katika matendo mema.^c

15 Endelea kusema mambo haya na kuhimiza* na kukaripia kwa mamlaka kamili.^d Usiache mtu yeyote akudharau.

3 Endelea kuwakumbusha wajitiishe na kuzitii serikali na mamlaka,^e wawe tayari kwa ajili ya kila kazi njema, **2** wasiseme vibaya kumhusu yeyote, wasiwe wagomvi, bali wawe na usawaziko,^f wakionyesha upole wote kwa watu wote.^g **3** Kwa maana hata sisi wakati mmoja tulikuwa watu wasio na akili, wasiotii, waliopotoshwa, watumwa wa tamaa na anasa mbalimbali, tukiendeleza ubaya na wivu, tukiwa wenye kuchukiza, na kuchukiana.

4 Hata hivyo, fadhili za Mwokozi wetu, Mungu,^h na upendo wake kwa wanadamu ulipofunuliwa, **5** (si kwa sababu ya matendo yoyote ya uadilifu tuliyo kuwa tumefanya,ⁱ bali kwa sababu ya rehema yake),^j alituokoa kupitia kuoshwa kulikutuleta kwenye uzima,^k na kwa kutufanya wapa kupitia roho takatifu.^l **6** Aliimimina roho hii kwa wingi* juu yetu kupitia Yesu Kristo Mwokozi wetu,^m **7** ili baada ya kutangazwa kuwa waadilifu kupitia fadhili zake zisizostahiliwa,ⁿ sisi tuwe warithi^o kulingana na tumaini la uzima wa milele.^p

2:14 *Tnn., "atutolee fidia; atukomboe."

2:15 *Au "kutia moyo." 3:6 *Au "kwa ukarimu."

8 Maneno haya ni yenye kutegemeka, na ninataka uendeleo kuyakazia mambo haya, ili wale ambao wamemwamini Mungu waendeleo kukaza fikira zao katika kudumisha matendo mema. Mambo haya ni mema na yanawanu-faisha watu.

9 Lakini epuka mabishano ya kipumbavu na kubishana kuhusu ukoo na mizozo na mapambano kuhusu Sheria, kwa maana mambo hayo hayana faida na ni ya ubatili.^a

10 Kuhusu mtu anayeendeleza madhehebu,^b mwepukeni^c baada ya kumwonya* mara ya kwanza na ya pili,^d 11 kwa kuwa mtu kama huyo ameiacha njia na anafanya dhambi, naye amejihukumu.

3:10 *Au "kumkemea."

SURA YA 3

a 1Ti 1:3, 4
1Ti 6:3-5

b 1Ko 11:19
Ufu 2:6

c Ro 16:17
2Yo 10

d 2Ti 4:2

Safu ya 2

a Mdo 20:4
Efe 6:21
2Ti 4:12

b 1Ko 9:14
Gal 6:6
Ebr 13:16

c 1Ko 9:11

d Kol 1:10

12 Nitakapomtuma Artema au Tikiko^a kwako, jitahidi kuja Nikopoli unione, kwa maana nimeamua kukaa huko majira ya baridi kali. 13 Jitahidi kabisa kuwapa Zena, aliye na ujuzi wa Sheria, na Apollo vitu wanavyohitaji ili wasikose kitu chochote kwa ajili ya safari yao.^b 14 Lakini acha watu wetu pia wajifunze kuendelea kufanya matendo mema ili wasaidie kunapokuwa na uhitaji wa dharura,^c ili wasikose kuzaa matunda.^{*d}

15 Wote walio pamoja nami wanakusalimu. Wape salamu zangu wale wanaotupenda katika imani.

Fadhili zisizostahiliwa za Mungu na ziwe pamoja nanyi nyote.

3:14 *Au "kupata matokeo mazuri."

KWA

FILEMONI

YALIYOMO

Salamu (1-3)

Upendo na imani ya Filemoni (4-7)

Paulo amsihi Filemoni kwa ajili ya

Onesimo (8-22)

Salamu za mwisho (23-25)

1 Paulo, mfungwa^a kwa ajili ya Kristo Yesu, na Timotheo^b ndugu yetu, kwa Filemoni mfanyakazi mwenzetu mpendwa, 2 na kwa Afia dada yetu, na kwa Arkipo^c mwanajeshi mwenzetu, na

a Efe 4:1

b Mdo 16:1, 2
Ebr 13:23

c Kol 4:17

Safu ya 2

a Ro 16:5
1Ko 16:19

kwa kutaniko lililo katika nyumba yako:^a

3 Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani kuto-ka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

4 Sikuzote ninamshukuru Mungu wangu ninapokutaja katika sala zangu,^a **5** ninaoendelea kusikia kuhusu imani na upendo wako kwa* Bwana Yesu na kwa* watakatifu wote. **6** Ninasali kwamba imani unayoshiriki na wengine ikuchochee kutambua kila jambo jema tulilo nalo kupitia Kristo. **7** Kwa maana nilipata shangwe nyingi na faraja niliposikia kuhusu upendo wako, kwa sababu wewe ndugu umeburudisha mioyo ya watakatifu.*

8 Kwa sababu hiyo, ingawa nina uhuru mkubwa wa ku-sema kuhusiana na Kristo wa kukuagiza ufanye jambo linalofaa, **9** ni afadhali nikusihi kwa msingi wa upendo, kwa kuwa mimi Paulo ni mwana-mume mzee, ndiyo, sasa pia ni mfungwa kwa ajili ya Kristo Yesu. **10** Ninakusihi kwa ajili ya mwanangu Onesimo,^b ambaye nimekuwa baba yake^c nikiwa gerezani.* **11** Zamani hakukufaa kitu, lakini sasa ni mwenye faida kwako na kwangu pia. **12** Ninamrudisha kwako, ndiyo yeye, moyo wangu mwenyewe.*

13 Ningependa akae nami hapa, ili achukue nafasi yako katika kunihudumia nikiwa nimefungwa kwa ajili ya habari njema.^d **14** Lakini sitaki kufanya jambo lolote bila ruhusa yako, ili ufanye tendo lako jema kwa hiari, bali si

5 *Au "kuelekea" 7 *Au "upendo mwororo wa watakatifu." 10 *Tnn., "katika vifungo." 12, 20 *Au "upendo wangu mwororo."

a Efe 1:15, 16
1Th 1:2

b Kol 4:9

c 1Ko 4:15

d Efe 6:19, 20
Flp 1:7

Safu ya 2

a 2Ko 9:7

b 1Ko 7:22

c 1Ti 6:2

d Flp 2:24

e Kol 1:7
Kol 4:12, 13

f Mdo 19:29
Mdo 27:2
Kol 4:10

g 2Ti 4:10

h Kol 4:14

kwa kulazimishwa.^a **15** Kwa kweli, labda ndiyo sababu alitoroka kwa muda mfupi,* ili arudi kwako milele, **16** si akiwa mtumwa tena,^b bali zaidi ya mtumwa, akiwa ndugu mpendwa,^c hasa kwangu, lakini hata zaidi kwako katika mwili na katika Bwana. **17** Kwa hiyo, ikiwa unaniona mimi kuwa rafiki yako,* mpokee kwa fadhili jinsi ambavyo ungenipokea mimi. **18** Zaidi ya hayo, ikiwa alikuko-sea au ana deni lako, basi nidai mimi. **19** Mimi Paulo ninaandika kwa mkono wangu mwenyewe: Nitakulipa—silitaji kukukumbusha kwamba hata wewe una deni langu, yaani, uhai wako mwenyewe. **20** Ndiyo, ndugu, ninaomba unisaidie jambo hili katika Bwana; burudisha moyo wangu* kuhusiana na Kristo.

21 Ninakuandikia nikiwa na uhakika kwamba utakubali, nikijua utafanya hata zaidi ya jambo ninalokuomba. **22** Lakini pamoja na hayo, pia nitayarishie makao, kwa maana ninatumaini kwamba kupitia sala zenu nitarudishwa kwenu.*^d

23 Epafra^e mfungwa mwenzangu katika muungano na Kristo Yesu anakusalimu, **24** pia wafanyakazi wenzangu Marko, Aristarko,^f Dema,^g na Luka.^h

25 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana Yesu Kristo na ziwe na roho mnayoonyesha.

15 *Tnn., "saa moja." 17 *Tnn., "mshiriki wako." 22 *Au "nitawekwa huru kwa ajili yenu."

KWA
WAEBRANIA

YALIYOMO

- 1 Mungu azungumza kupitia Mwana wake (1-4)
Mwana ni mkuu kuliko malaika (5-14)
- 2 Kazia uangalifu zaidi kuliko ilivyo kawaida (1-4)
Vitu vyote vimetiishwa kwa Yesu (5-9)
Yesu na ndugu zake (10-18)
Wakili Mkuu wa wokovu wao (10)
Kuhani mkuu mwenye rehema (17)
- 3 Yesu ni mkuu kuliko Musa (1-6)
Vitu vyote vilitengenezwa na Mungu (4)
Onyo dhidi ya kukosa imani (7-19)
"Leo ikiwa mtaisikiliza sauti yake" (7, 15)
- 4 Hatari ya kutoingia katika pumziko la Mungu (1-10)
Himizo la kuingia katika pumziko la Mungu (11-13)
Neno la Mungu liko hai (12)
Yesu, kuhani mkuu aliye bora (14-16)
- 5 Yesu ni mkuu kuliko makuhani wakuu wanadamu (1-10)
Kwa mfano wa Melkizedeki (6, 10)
Alijifunza utii kutokana na mateso (8)
Ana daraka la kuleta wokovu wa milele (9)
Onyo dhidi ya kukosa ukomavu (11-14)
- 6 Kusonga mbele kuelekea ukomavu (1-3)
Wale wanaoanguka wanamtundika tena Mwana kwenye mti (4-8)
Fanyeni tumaini lenu kuwa hakika (9-12)
Uhakika wa ahadi ya Mungu (13-20)
Ahadi na kiapo cha Mungu havibadiliki (17, 18)
- 7 Melkizedeki, mfalme na kuhani wa pekee (1-10)
Ubora wa ukuhani wa Kristo (11-28)
Kristo anaweza kuokoa kikamili (25)
- 8 Maskani iliwakilisha vitu vya mbinguni (1-6)
Tofauti kati ya agano la kale na agano jipya (7-13)
- 9 Utumishi mtakatifu katika hekalu la duniani (1-10)
Kristo aingia mbinguni akiwa na damu yake (11-28)
Mpatanishi wa agano jipya (15)
- 10 Dhabihu za wanyama haziwezi kuondoa dhambi (1-4)
Sheria ni kivuli (1)
Dhabihu ya Kristo ilitolewa mara moja kwa wakati wote (5-18)
Njia mpya ya kuingia yenye uzima (19-25)
Tusiache kukutana pamoja (24, 25)
Onyo dhidi ya dhambi ya kimakusudi (26-31)
Uhakika na imani ili kuvumilia (32-39)
- 11 Maana ya imani (1, 2)
Mifano ya imani (3-40)
Haiwezekani kumpendeza Mungu bila imani (6)
- 12 Yesu, Mkamilishaji wa imani yetu (1-3)
Wingu kubwa la mashahidi (1)
Usiipuuze nidhamu ya Yehova (4-11)
Fanyia miguu yako mapito yaliyonyooka (12-17)
Kukaribia Yerusalemu la mbinguni (18-29)
- 13 Himizo na salamu za kumalizia (1-25)
Msisahau kuwakaribisha wageni (2)
Ndoa na iheshimiwe (4)
Watiini wale wanaoongoza (7, 17)
Kutoa dhabihu ya sifa (15, 16)

1 Zamani za kale, Mungu alizungumza na mababu zetu kupitia manabii katika pindi nyingi na kwa njia nyingi.^a

2 Lakini sasa mwishoni mwa siku hizi amezunguza nasi kupitia Mwana,^b aliyemweka rasmi kuwa mrithi wa vitu vyote,^c na kupitia kwake alifanya mifumo ya mambo.*^d

3 Yeye ndiye mng'ao wa utukufu wa Mungu^e na mfano kamili wa utu wake,^f naye hutegemeza vitu vyote kwa neno la nguvu zake. Na baada ya kuzitakasa dhambi zetu,^g aliketika kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko juu.^h **4** Kwa hiyo amekuwa bora kuliko malaika,ⁱ kwa maana amerithi jina bora kabisa kuliko lao.^j

5 Kwa mfano, Mungu aliwahi kumwambia nani kati ya malaika: "Wewe ni mwanangu; leo nimekuwa baba yako"?^k Na tena: "Nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu"?^l

6 Lakini anapomleta tena Mzaliwa wake wa kwanza^m katika dunia inayokaliwa, anasema: "Malaika wote wa Mungu na wamsujudie."*

7 Pia, anasema kuhusu malaika: "Huwafanya malaika wake kuwa roho, na wahudumu wakeⁿ kuwa mwali wa moto."^o **8** Lakini kumhusu Mwana, anasema: "Mungu ni kiti chako cha ufalme^p milele na milele, na fimbo ya Ufalme wako ni fimbo ya unyoofu.*

9 Ulipenda uadilifu, nawe ukachukia uasi sheria. Ndiyo sababu Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta^q kwa mafuta ya kushangilia kuliko wenza-

1:2 * Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo." 1:6 * Au "wamwinamie." 1:7 * Au "watumishi wake wa watu wote." 1:8 * Au "haki."

SURA YA 1

a Kut 24:3

Hes 12:8

Yer 7:25

b Mt 17:5

c Zb 2:8

d Yoh 1:3

1Ko 8:6

Kol 1:16

e Yoh 1:14

Yoh 17:5

f Kol 1:15

g Ebr 9:26

h Zb 110:1

Mdo 2:32, 33

Mdo 7:55

i Efe 1:20, 21

1Pe 3:22

j Mdo 4:12

Flp 2:9, 10

k Zb 2:7

l 2Sa 7:14

Mk 1:11

Lu 9:35

2Pe 1:17

m Yoh 1:14

Ro 8:29

Kol 1:15

n Zb 91:11

Lu 22:43

o Zb 104:4

p Mt 28:18

Ufu 3:21

q Isa 61:1

Lu 3:21, 22

Lu 4:18

m Mdo 5:18, 19

n Mdo 5:18, 19

o Mdo 5:18, 19

p Mdo 5:18, 19

q Mdo 5:18, 19

r Mdo 5:18, 19

s Mdo 5:18, 19

t Mdo 5:18, 19

u Mdo 5:18, 19

v Mdo 5:18, 19

w Mdo 5:18, 19

x Mdo 5:18, 19

y Mdo 5:18, 19

z Mdo 5:18, 19

aa Mdo 5:18, 19

ab Mdo 5:18, 19

ac Mdo 5:18, 19

ad Mdo 5:18, 19

ae Mdo 5:18, 19

af Mdo 5:18, 19

ag Mdo 5:18, 19

ah Mdo 5:18, 19

ai Mdo 5:18, 19

aj Mdo 5:18, 19

ak Mdo 5:18, 19

al Mdo 5:18, 19

am Mdo 5:18, 19

an Mdo 5:18, 19

ao Mdo 5:18, 19

ap Mdo 5:18, 19

aq Mdo 5:18, 19

ar Mdo 5:18, 19

as Mdo 5:18, 19

at Mdo 5:18, 19

au Mdo 5:18, 19

av Mdo 5:18, 19

aw Mdo 5:18, 19

ax Mdo 5:18, 19

ay Mdo 5:18, 19

az Mdo 5:18, 19

ko."^a **10** Na: "Hapo mwanzoni, Ee Bwana, uliweka misingi ya dunia, na mbingu ni kazi za mikono yako. **11** Hizo zitaa-ngamia, lakini wewe utadumu; na zote zitachakaa kama vazi, **12** nawe utazikunja kama kanzu, kama vazi, nazo zitabandilishwa. Lakini wewe ni yule yule, na miaka yako haitafikia mwisho kamwe."^b

13 Lakini amewahi kumwambia malaika yupi hivi: "Keti kwenye mkono wangu wa kuume mpaka niwaweke maddui wako kuwa kiti cha miguu yako"?^c **14** Je, wao wote si roho kwa ajili ya utumishi mtakatifu,^{*d} waliotumwa kuhudumu kwa ajili ya wale wataorithi wokovu?

2 Hiyo ndiyo sababu ni lazima tuyakazie uangalifu zaidi kuliko ilivyo kawaida mambo tuliyosikia,^e ili tusipeperushwe kamwe.^f **2** Kwa maana ikiwa neno lililosemwa kupitia malaika^g lilikuwa hakika, na kila kosa na tendo la kutotii liliadhibiwa kupatana na haki,^h **3** je, sisi tutaponyoka ikiwa tumepuza wokovu huo mkuu?ⁱ Kwa kuwa ulianza kusemwa kupitia Bwana wetu^j nasi tukathibitishiwa na wale waliomsikia, **4** huku Mungu akijiunga katika kutoa ushahidi kwa ishara na mambo ya ajabu^{*} na matendo mbalimbali yenye nguvu^k na roho takatifu iliyotolewa kulingana na mapenzi yake.^l

5 Kwa maana dunia inayokaliwa inayokuja,^m ambayo tunazunguma kuhusu hajaitiisha chini ya malaika. **6** Lakini mahali fulani shahidi

1:14 * Au "utumishi wa watu wote." 2:4 * Au "miujiza."

mmoja alisema: “Mwanadamu ni nini hivi kwamba unamweka akilini, au mwana wa mtu hivi kwamba unamtunza?”^a **7** Ulimfanya awe mdogo kidogo kuliko malaika; ulimvika taji kwa utukufu na heshima, na kumweka juu ya kazi za mikono yako. **8** Ulivitiisha vitu vyote chini ya miguu yake.”^b Kwa kuvitiisha vitu vyote chini yake,^c Mungu hakuacha kitu chochote kisichotiishwa chini yake.^d Ingawa hivyo, bado hatuoni vitu vyote vikiwa vi-metiishwa chini yake.^e **9** Lakini tunamwona Yesu, ali-yafanywa kuwa mdogo kidogo kuliko malaika,^f sasa amevikwa taji la utukufu na heshima kwa kupatwa na kifo,^g ili kwa fadhili zisizostahiliwa za Mungu aonje kifo kwa ajili ya kila mtu.^h

10 Kwa maana ilifaa kwa mba yule ambaye kwa ajili yake na kupitia kwake vitu vyote vipo, katika kuleta wana wengi kwenye utukufu,ⁱ alipaswa kumfanya Wakili Mkuu wa wokovu wao/ awe mkamilifu kupitia mateso.^k **11** Kwa maana yule anayetakasa na wale wanaotakaswa^l pia wote hutokana na mmoja,^m na kwa sababu hiyo yeye haoni aibu kuwaita ndugu,ⁿ **12** kama anavyosema: “Nitalitangaza jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kutaniko nitakusifu kwa wimbo.”^o **13** Na tena: “Nitamtegemea yeye.”^p Na tena: “Tazama! Mimi na wato wadogo, ambao Yehova* alinipa.”^q

14 Basi, kwa kuwa “wato wadogo” ni washiriki wa damu na mwili, vivyo hivyo yeye pia aliyashiriki mambo

2:13 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 2

a Zb 144:3
b Zb 8:4-6
c Mt 28:18
1Ko 15:27
Efe 1:22
d 1Pe 3:22
e Zb 110:1
f Flp 2:7
g Ufu 5:9
h Isa 53:5,8
Ro 5:17
1Ti 2:5,6
i Ro 8:18,19
2Ko 6:18
j Mdo 5:31
Ebr 12:2
k Lu 24:26
Ebr 5:8
l Yoh 17:19
Ebr 10:14
m Yoh 20:17
n Mt 12:50
Ro 8:29
o Zb 22:22
p Isa 8:17
q Isa 8:18

Safu ya 2

a Yoh 1:14
b Ayu 1:19
c Mwa 3:15
Lu 10:18
Yoh 8:44
1Yo 3:8
Ufu 12:9
d Isa 25:8
Ro 8:20, 21
1Ko 15:26
e Gal 3:29
f Flp 2:7
g Ro 3:25
1Yo 2:1, 2
1Yo 4:10
h Ro 5:10
i Ebr 4:15
j Ebr 7:25
Ufu 3:10

SURA YA 3

k Flp 3:14
1Th 2:12
l Ebr 8:1
m Yoh 8:29
n Hes 12:7
o Mt 17:1, 2

hayo,^a ili kupitia kifo chake amwangamize yule aliye na uwezo wa kusababisha kifo,^b yaani, Ibilisi,^c **15** na ili awe-weke huru* wale wote walio-kuwa chini ya utumwa katika maisha yao yote kwa kuogopa kifo.^d **16** Kwa maana kwa kweli yeye hawasaidii malaika, bali anasaidia uzao wa* Abrahamu.^e **17** Kwa hiyo alipaswa kuwa kama “ndugu” zake katika mambo yote,^f ili awe kuhani mkuu mwenye rehema na mwaminifu katika mambo yanayohusiana na Mungu, ili atoe dhahihu ya upatanisho*^g kwa ajili ya dhambi za watu.^h **18** Kwa kuwa yeye mwenyewe aliteseka alipokuwa akijaribiwa,ⁱ anaweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa.^j

3 Kwa hiyo, ndugu watakatifu, washiriki wa mwito* wa mbinguni,^k mfikirieni mtume na kuhani mkuu tunayemkubali*—Yesu.^l **2** Alikuwa mwaminifu kwa Yule aliyemchagua,^m kama vile Musa alivyokuwa pia katika nyumba yote ya Mungu.ⁿ **3** Kwa maana huyo* anastahili utukufu zaidi^o kuliko Musa, kwa kuwa yule anayejenga nyumba ana heshima kuliko nyumba yenyewe. **4** Bila shaka, kila nyumba hujengwa na mtu fulani, lakini yule aliyevijenga vitu vyote ni Mungu. **5** Sasa Musa alikuwa mtumishi mwaminifu katika nyumba yote ya Huyo akiwa usuhuda* wa mambo ambayo yange-semwa baadaye, **6** lakini Kristo alikuwa mwaminifu aki-

2:15 *Au “awakomboe.” 2:16 *Tnn., “mbegu ya.” 2:17 *Au “atoe dhahihu ya kufunika dhambi; kufunika dhambi.” 3:1 *Au “mwaliko.” #Au “tunayemkiri.” 3:3 *Yaani, Yesu. 3:5 *Au “ushahidi.”

wa mwana^a juu ya nyumba ya Mungu. Sisi ni nyumba Yake,^b ikiwa kwa kweli tunashikilia imara uhuru wetu wa kusema na tumaini ambalo tunajisifia mpaka mwisho.

7 Kwa hiyo, kama vile roho takatifu navyosema,^c "Leo ikiwa mtaisikiliza sauti yake, **8** msiifanye mioyo yenu kuwa migumu kama ule wakati wa kusababisha hasira kali, kama siku ile ya jaribu nyikani,^d **9** ambayo mababu zenu wali-niweka kwenye jaribu, na kunipima, ingawa waliona matendo yangu kwa miaka 40.^e **10** Ndiyo sababu nilichukizwa na kizazi hiki, nikasema: 'Wao hupotoka sikuzote katika mioyo yao, nao hawazijui njia zangu.' **11** Kwa hiyo niliapa kwa hasira yangu: 'Hawataingia katika pumziko langu.'"^f

12 Jihadharini, akina ndugu, ili moyo mwovu unaokosa imani usisitawi ndani ya yeyote kati yenu kwa kujiondoa kwa Mungu aliye hai;^g **13** lakini endeleeni kutiana moyo kila siku, maadamu inaitwa "Leo,"^h ili yeyote kati yenu asifanywe kuwa mgumu kwa nguvu za udanganyifu za dhambi. **14** Kwa maana kwa kweli tunakuwa washiriki wa* Kristo ikiwa tu tunashikilia imara mpaka mwisho uhakika tuliokuwa nao mwanzoni.ⁱ **15** Kama inavyosemwa, "Leo ikiwa mtaisikiliza sauti yake, msiifanye mioyo yenu kuwa migumu kama ule wakati wa kusababisha hasira kali."^j

16 Kwa maana ni nani waliosikia na bado wakamchochea kuwa na hasira kali?

3:14 *Au "tunakuwa na ushirika na."

SURA YA 3

a Mt 17:5

b 1Pe 2:5

c 2Sa 23:2
Mdo 1:16

d Kut 17:7

e Kut 16:35
Hes 32:13
Zb 95:9f Hes 14:22, 23
Zb 95:7-11

g Ebr 2:1

h Zb 95:7

i Ufu 2:10

j Zb 95:7, 8

Safu ya 2

a Kut 17:1-3
Hes 14:2, 4b Hes 14:11
Kum 32:21c Hes 14:22, 23
Hes 14:28-30
Yud 5

d Ebr 4:6

SURA YA 4

e Ebr 3:12, 13

f Mt 4:23
Mdo 15:7
Kol 1:23g Zb 95:11
Ebr 3:11

h Kut 31:17

i Mwa 2:2, 3

j Zb 95:11

k Hes 14:30
Kum 31:27

Kwa kweli, je, si wale wote waliotoka Misri chini ya Musa?^a **17** Zaidi ya hayo, Mungu alichukizwa na akina nani kwa miaka 40?^b Je, si wale waliotenda dhambi, ambao maiti zao zilianguka nyikani?^c **18** Naye aliapa kwa akina nani kwamba hawataingia katika pumziko lake? Je, si wale waliotenda kwa kutotii? **19** Kwa hiyo tunaona kwamba hawakuingia kwa sababu walikosa imani.^d

4 Kwa hiyo, kwa kuwa aha-di ya kuingia katika pumziko lake bado ipo, acheni tuwe macho* ili yeyote kati yenu asionekane amepungukiwa.^e **2** Kwa maana sisi pia tumetangaziwa habari njema,^f kama walivyotangaziwa; lakini neno walilosikia halikuwaletea faida, kwa sababu hawakuunganishwa kwa imani pamoja na wale waliosikia. **3** Kwa maana sisi ambao tumeonyesha imani tunaingia katika pumziko, kama alivyosema: "Kwa hiyo niliapa kwa hasira yangu, 'Hawataingia katika pumziko langu,'"^g ingawa kazi zake zilimalizika tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.^h **4** Kwa maana mahali fulani amesema hivi kuhusu siku ya saba: "Na Mungu akapumzika siku ya saba kutoka katika kazi zake zote."ⁱ **5** na hapa tena anasema: "Hawataingia katika pumziko langu."^j

6 Basi, kwa kuwa bado imebaki watu fulani waingie katika pumziko hilo, na wale ambao walitangaziwa kwanzia habari njema hawakuingia kwa sababu ya kutotii,^k **7** yeye tena anaweka siku fulani kwa kusema baadaye katika zaburi ya Daudi, "Leo";

4:1 *Tnn., "tuwe na woga."

kama ilivyosemwa hapo juu, “Leo ikiwa mtaisikiliza sauti yake, msiifanye mioyo yenu kuwa migumu.”^a **8** Kwa maana ikiwa Yoshua^b aliwaingiza katika mahali pa pumziko, Mungu hangesema baadaye kuhusu siku nyingine. **9** Kwa hiyo bado limebaki pumziko la sabato kwa ajili ya watu wa Mungu.^c **10** Kwa maana mtu ambaye ameingia katika pumziko la Mungu, amepumzika pia kutoka kwenye kazi zake mwenyewe, kama Mungu alivyopumzika kutoka kwenye kazi zake.^d

11 Kwa hiyo acheni tufanye yote tunayoweza ili kuingia katika pumziko hilo, ili yeyote asije akaanguka katika kielelezo kilekile cha kutotii.^e **12** Kwa maana neno la Mungu liko hai nalo ni lenye nguvu^f na lina makali kuliko upanga wowote wenye makali pande mbili^g nalo huchoma hata kufikia kugawanya nafsi* na roho,* na viungo kutoka katika urojorojo, nalo linaweza kutambua fikira na makusudio ya moyo. **13** Na hakuna kiumbe kilichofichwa machoni pake,^h bali vitu vyote viko uchi navyo vimefunuliwa wazi machoni pa yule ambaye tunapaswa kutoa hesabu kwake.ⁱ

14 Basi, kwa kuwa tuna kuhani mkuu sana ambaye ameingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu,^j acheni tundelee kumtangaza hadharani.^k **15** Kwa maana hatuna kuhani mkuu ambaye hawezi kuusikitikia udhaifu wetu,^l bali tuna yule ambaye amejaribiwa katika mambo yote kama tulivyojaribiwa, lakini hakutenda dhambi.^m **16** Basi

SURA YA 4

a Zb 95:7, 8

b Kut 24:13
Kum 1:38

c Mk 2:28

d Mwa 2:2, 3

e Zb 95:11

f Yer 23:29
1Th 2:13

g Efe 6:17

h Zb 7:9
Zb 90:8
Met 15:11i Mdo 17:31
Ro 2:16
Ro 14:12

j Mk 1:11

k Ebr 10:23

l Isa 53:4
Ebr 2:17m Ebr 7:26
1Pe 2:22

Safu ya 2

a Efe 3:11, 12
Ebr 10:19-22

SURA YA 5

b Kut 40:13

c Law 5:6

d Law 9:7
Law 16:6

e Kut 28:1

f Yoh 8:54

g Zb 2:7
Mdo 13:33

h Zb 110:4

i Lu 22:44
Yoh 12:27

na tukikaribie kiti cha ufalme cha fadhili zisizostahiliwa tu kiwa na uhuru wa kusema,^a ili tupokee rehema na kupata fadhili zisizostahiliwa tunapohitaji msaada.*

5 Kwa maana kila kuhani mkuu anayechaguliwa miogoni mwa wanadamu huwekwa rasmi kwa ajili yao juu ya mambo yanayohusiana na Mungu,^b ili atoe zawadi na dhabihu kwa ajili ya dhambi.^c **2** Yeye anaweza kuwate ndea kwa huruma* wale wasiojua na wanaokosea,^d kwa sababu yeye pia anapambana^e na udhaifu wake mwenyewe, **3** na hivyo ni lazima atoe dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe kama vile anavyotoa kwa ajili ya dhambi za watu.^d

4 Mtu hapati heshima hii kwa kupenda kwake mwenyewe, bali huipokea tu Mungu anapomwita, kama Haruni alivyoitwa.^e **5** Vivyo hivyo, pia Kristo hakujitukuza mwenyewe^f kwa kuwa kuhani mkuu, bali alitukuzwa na Yule aliymwambia hivi: “Wewe ni mwangu; leo nimekuwa baba yako.”^g **6** Kama vile pia anavyosema mahali pengine, “Wewe ni kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki.”^h

7 Alipokuwa duniani,* Kristo alitoa dua na pia maombi, kwa vilio vyenye nguvu na machozi,ⁱ kwa Yule aliyekuwa na uwezo wa kumwokoza kutoka katika kifo, naye akasikilizwa vizuri kwa sababu ya kumwogopa Mungu. **8** Ingawa alikuwa mwana, alijifunza ku-

4:16 *Au “zitusaidie wakati unaofaa.”
5:2 *Au “kwa wororo; kwa kiasi.”
5:7 *Au “wasiotii.”
5:7 *Au “anakabiliana.”
5:7 *Tnn., “Katika siku za mwili wake.”

tii kutokana na mateso yaliyom-pata.^a **9** Na baada ya kufanywa kuwa mkamilifu,^b akawa na daraka la wokovu wa milele kwa ajili ya wote wanao-
mtii,^c **10** kwa sababu Mungu amemteua kuwa kuhani mkuu kwa mfano wa Melkizedeki.^d

11 Tuna mengi ya kusema kumhusu na ni vigumu kuyafafanua, kwa sababu mme-
kuwa wazito wa kusikia. **12** Kwa maana, ingawa kufikia sasa* mnapaswa kuwa walimu, mnahitaji tena mtu awafundishe tangu mwanzo mambo ya msingi^e ya maneno matakatifu ya Mungu, nanyi mnahitaji maziwa tena, bali si chakula kigumu. **13** Kwa kuwa kila mtu anayeendelea kunywa maziwa hafahamu neno la uadilifu, kwa maana yeye ni mtoto mdogo.^f **14** Lakini chakula kigumu ni cha watu wakomavu, ambao wamezoeza nguvu zao za utambuzi* kwa kuzitumia ili kutofautisha mambo yaliyo sawa na mambo yasiyo sawa.

6 Kwa hiyo, kwa kuwa sasa tumeliacha nyuma fundisho la msingi^g kumhusu Kristo, na tusonge mbele kuelekea ukomavu,^h tusiweke msingi tena, yaani, kutubu matendo yaliyokufa na imani katika Mungu, **2** fundisho kuhusu aina mbalimbali za ubatizo na kuweka mikono,ⁱ kufufuliwa kwa wafu/ na hukumu ya milele. **3** Na tutafanya hivyo ikiwa kwa kweli Mungu ataruhusu.

4 Kwa maana kuhusu wale ambao wakati fulani walikuwa kwenye nuru,^k na ambao wameonja zawadi ya bure ya

5:12 *Tnn., "kulingana na wakati."
5:14 *Au "nguvu zao za ufahamu."

SURA YA 5

a Mt 26:39
Flp 2:8

b Ebr 7:28

c Yoh 3:16

d Zb 110:4

e Ebr 6:1

f Efe 4:14

SURA YA 6

g Ebr 5:12

h 1Ko 14:20
Efe 4:13
Ebr 5:14

i Mdo 8:17

j Mt 22:31
Yoh 5:28, 29
Yoh 11:25

k Efe 1:18
Ebr 10:26

Safu ya 2

a 1Yo 2:19

b Ebr 10:29

c Ebr 10:32, 33

d 1Pe 1:3, 4

e Ebr 3:14

f Ro 12:11
Ufu 2:4

g Mwa 22:16

h Mwa 22:17

kimbingu na ambao wamekuwa washiriki wa roho takatifu **5** na ambao wameonja neno zuri la Mungu na nguvu za mfumo wa mambo* unaokuja, **6** lakini wameanguka,^a haiwezekani kuwarudisha tena kwenye toba, kwa sababu wanamtundika tena mtini Mwana wa Mungu kwa ajili yao wenyewe na kumwaibisha hadharani.^b **7** Kwa maana udongo hupokea baraka kutoka kwa Mungu unapokunywa mvua inayonyesha juu yake mara kwa mara, na kisha huzaa mimea inayowanufaisha wale wanaoulima. **8** Lakini ukizaa miiba na michongoma, hukataliwa na huwa karibu kulaaniwa, na mwishowe huchomwa.

9 Lakini wapendwa, ingawa tunazungumza hivyo, tuna hakika mna hali bora, yaani, hali inayohusiana na wokovu. **10** Kwa maana Mungu hakosi kuwa mwadilifu hivi kwamba asahau kazi yenu na upendo mlioonyesha kwa ajili ya jina lake,^c kwa kuhudumu na kuendelea kuwahudumia watakatifu. **11** Lakini tunatamani kila mmoja wenu awe na bidii ileile ili kuwa na uhakikisho kamili wa tumaini^d mpa-
ka mwisho,^e **12** ili msiwe goigoi,^f bali muwe waigaji wa wale ambao kupitia imani na subira huzirithi ahadi.

13 Kwa maana Mungu alipotoa ahadi yake kwa Abrahamu, kwa kuwa hangeweza kuapa kwa yeyote aliye mkubwa zaidi, aliapa kwa jina lake mwenyewe,^g **14** akisema: "Hakika nitakubariki nami hakika nitaufanya uzao wako uwe mwingi."^h **15** Basi, baada ya

6:5 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

Abrahamu kuonyesha subira, aliipata ahadi hiyo. **16** Kwa maana watu huapa kwa mtu aliye mkubwa zaidi yao, na kiapo chao ndicho mwisho wa kila bishano, kwa kuwa ndicho uhakikisho wao wa kishe-ria.^a **17** Vivyo hivyo, Mungu alipoamua kuwaonyesha waziwazi warithi wa ile ahadi^b jinsi kusudi* lake lisivyobadilika, alitoa uhakikisho[#] kwa kiapo, **18** ili kupitia mambo mawili yasiyobadilika ambayo kuhusiana nayo Mungu hawezi kamwe kusema uwongo,^c sisi ambao tumekimbia kwenda katika kimbilio tutiwe moyo kabisa ili tushike imara tumaini lililowekwa mbele yetu. **19** Tuna tumaini hilo^d kama nanga ya nafsi,* likiwa hakika na imara, nalo huingia ndani ya pazia,^e **20** ambamo mtangulizi ameingia kwa ajili yetu, Yesu,^f ambaye amekuwa kuhani mkuu milele kama Melkizedeki.^g

7 Kwa maana huyu Melkizedeki, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu Aliye Juu Zaidi, alikutana na Abrahamu akirudi baada ya kuwaangamiza wafalme kisha akambariki,^h **2** naye Abrahamu akampa* sehemu ya kumi ya vitu vyote. Kwanza, jina lake linatafsiriwa "Mfalme wa Uadilifu," kisha pia mfalme wa Salemu, yaani, "Mfalme wa Amani." **3** Hana baba wala mama, hana ukoo, na hana mwanzo wa siku wala mwisho wa uzima, bali akiwa amefanywa kama Mwana wa Mungu, anadumu akiwa kuhani daima.*ⁱ

6:17 *Au "shauri." #Au "aliingilia kati." Tnn., "alifanya upatanisho." 6:19 *Au "ya uhai wetu." 7:2 *Tnn., "akamgawia." 7:3 *Au "kwa wakati wote."

SURA YA 6

a Mwa 31:53

b Gal 3:29

c Hes 23:19
Tit 1:2

d 1Pe 1:3, 4

e Law 16:2, 12
Ebr 9:7
Ebr 10:19, 20

f Ebr 4:14

g Zb 110:4
Ebr 5:6

SURA YA 7

h Mwa 14:17-20

i Zb 110:4

Safu ya 2

a Mwa 14:20

b Kut 40:12, 15

c Hes 18:21, 26
Kum 14:28d Mwa 12:7
Mwa 14:18-20
Mwa 17:6
Mwa 22:17

e Ebr 7:3

f Mwa 14:18

g Ro 3:20
Ebr 7:19
Ebr 9:9
Ebr 10:1

h Zb 110:4

4 Oneni jinsi mtu huyu alivyokuwa mkuu, ambaye Abrahamu yule kichwa cha familia,* alimpa sehemu ya kumi kutoka kwa zile nyara bora.^a

5 Ni kweli, kulingana na Sheria, wazao wa Lawi^b ambao hupokea cheo chao cha ukuhani, wana amri ya kukusanya sehemu za kumi kutoka kwa watu,^c yaani, kutoka kwa ndugu zao, ingawa hao ni wazao wa* Abrahamu. **6** Lakini mtu huyu ambaye ukoo wake haukutokana nao, alichukua sehemu za kumi kutoka kwa Abrahamu na kumbariki yule aliyekuwa na zile ahadi.^d

7 Basi hakuna shaka kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa. **8** Na kwa upande mmoja, watu wanaokufa ndio wanaopokea sehemu za kumi, lakini kwa upande mwingine, ni mtu ambaye ushahidi unatolewa kwamba anaishi.^e **9** Na inaweza kusemwa kwamba hata Lawi, ambaye hupokea sehemu za kumi, amelipa sehemu za kumi kupitia Abrahamu, **10** kwa maana bado alikuwa mzao wa wakati ujao wa* babu yake wakati Melkizedeki alipokutana naye.^f

11 Basi, ikiwa ukamilifu ungeweza kupatikana kupitia ukuhani wa Walawi^g (kwa maana ulikuwa sehemu ya Sheria ambayo watu walipewa), kungekuwa na umuhimu gani wa kuhani mwingine kusimama anayesemwa kuwa kwa mfano wa Melkizedeki^h na si kwa mfano wa Haruni? **12** Kwa kuwa ukuhani unabadilishwa, inakuwa muhimu kubadilisha She-

7:4 *Au "mzee wa ukoo." 7:5 *Tnn., "wametoka katika kiuno cha." 7:10 *Tnn., "katika kiuno cha."

ria pia.^a **13** Kwa maana mtu ambaye mambo haya yanasema kumhusu alitoka katika kabila lingine, na hakuna mtu wa kabila hilo ambaye amewahi kuhudumu kwenye madhabu.^b **14** Kwa kuwa ni wazi kwamba Bwana wetu ametokana na Yuda,^c naye Musa hakusema kwamba makuhani wangetoka katika kabila hilo.

15 Na hilo linakuwa wazi hata zaidi kuhani mwingine^d anaposimama ambaye ni kama Melkizedeki,^e **16** ambaye amekuwa hivyo, si kupitia matakwa ya kisheria yanayotegemea uzao wa kimwili, bali kupitia nguvu za uzima usioweza kuharibika.^f **17** Kwa maana imesemwa katika ushahidi kumhusu: "Wewe ni kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki."^g

18 Basi, ile amri ya zamani inawekwa kando kwa sababu ni dhaifu na haifai.^h **19** Kwa maana Sheria haikufanya kitu chochote kiwe kikamilifu,ⁱ lakini kuletwa kwa tumaini bora^j kulifanya hivyo, na kupitia tumaini hilo tunamkaribia Mungu.^k **20** Pia, kwa kuwa jambo hilo halikufanywa bila kiapo rasmi **21** (kwa kweli, kuna watu ambao wamekuwa makuhani bila kiapo rasmi, lakini huyu amekuwa kuhani kupitia kiapo kilichotolewa kumhusu na Yule aliyesema hivi: "Yehova* ameapa naye hatabadili nia yake,^l 'Wewe ni kuhani milele'"),ⁱ **22** kwa hiyo Yesu amekuwa uhakikisho* wa agano bora.^m **23** Zaidi ya hayo, wengi walikuwa makuhani mmoja baada ya mwingi-

7:21; 8:2 * Angalia Nyongeza A5. 7:21 * Au "hataghairi." 7:22 * Au "yule aliyewekwa kuwa rehani."

SURA YA 7

- a Ro 3:27
1Ko 9:21
Gal 6:2
Kol 2:13, 14
b Hes 18:6, 7
c Mwa 49:10
Mt 1:1, 3
Lu 3:23, 33
d Ebr 3:1
Ebr 7:26
e Zb 110:4
f Ro 6:9
1Ti 6:16
g Zb 110:4
h Ro 8:3
Ebr 9:9
Ebr 13:9
i Mdo 13:38, 39
Gal 2:15, 16
Ebr 10:1
j 1Pe 1:3, 4
k Yoh 14:6
Ebr 4:16
l Zb 110:4
m Yer 31:31
Mt 26:27, 28
1Ko 11:25
Ebr 8:6
Ebr 9:15
Ebr 12:22, 24

Safu ya 2

- a 1Nya 6:4
b Lu 1:33
Ebr 7:15, 16
c Ro 8:34
1Ti 2:5
Ebr 9:24
1Yo 2:1
d Isa 53:9
1Pe 2:21, 22
e Efe 1:20, 21
1Pe 3:22
f Hes 28:3
g Law 9:8, 15
h Ro 6:10
Ebr 9:28
Ebr 10:14
i Law 16:11
j Zb 2:7
Zb 110:4
k Ebr 2:10
Ebr 5:9

SURA YA 8

- l Ebr 3:1
Ebr 7:26
m Zb 110:1
Ebr 1:3
n Ebr 9:8, 24
o Efe 5:2

ne^a kwa sababu kifo kiliwaziwa wasiendelee kuwa makuhani, **24** lakini kwa sababu yeye anaendelea kuishi milele,^b hakuna anayerithi ukuhani wake. **25** Basi anaweza pia kuwaokoa kikamili wale wanaomkaribia Mungu kupitia yeye, kwa sababu sikuzote yuko hai ili kuwaombea.^c

26 Kwa maana inafaa tuwe na kuhani mkuu kama huyo ambaye ni mshikamanifu, asiye na hatia, asiye na unajisi,^d aliyetenganishwa na watenda dhambi, na aliyeinuliwa juu ya mbingu.^e **27** Tofauti na makuhani hao wakuu, hahitaji kutoa dhambi kila siku,^f kwanzwa kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe kisha kwa ajili ya dhambi za watu,^g kwa sababu alifanya hivyo mara moja kwa wakati wote alipojitoa mwenyewe.^h **28** Kwa maana Sheria huweka rasmi watu walio na udhaifu wawe makuhani wakuu,ⁱ lakini neno la kiapo^j rasmi baada ya Sheria humweka rasmi Mwana, ambaye amefanywa kuwa mkamilifu^k milele.

8 Sasa jambo kuu tunalosema ni hili: Sisi tuna kuhani mkuu wa namna hii,^l naye ameketi kwenye mkono wa kuume wa kiti cha ufalme cha Ukuu mbinguni,^m **2** mhudumuⁿ wa mahali patakatifuⁿ na wa hema la kweli, ambalo limesimamishwa na Yehova,^{*} na si mwanadamu. **3** Kwa maana kila kuhani mkuu huwekwa rasmi ili kutoa zawadi na dhabihu; basi ilikuwa lazima huyu pia awe na kitu cha kutoa.^o **4** Ikiwa angekuwa duniani, hangekuwa

8:2 * Au "mtumishi wa watu wote."

kuhani,^a kwa sababu tayari kuna watu wanaotoa zawadi kulingana na Sheria. **5** Watu hao hufanya utumishi mtakatifu kwa mfano wa uhalisi na kivuli^b cha vitu vya mbinguni;^c kama vile Musa, alipokuwa karibu kujenga hema, alipewa amri na Mungu: Kwa kuwa Mungu anasema: “Hakikisha kwamba unatengeneza vitu vyote kwa kufuata kielelezo ulichoonyeshwa mlimani.”^d **6** Lakini sasa Yesu amepata huduma iliyo bora* zaidi kwa sababu yeye pia ni mpatanishi^e wa agano lililo bora^f kwa kulinganishwa, ambalo limefanywa imara kisheria juu ya ahadi zilizo bora.^g

7 Ikiwa agano la kwanza halingekuwa na kosa, hakungekuwa na haja ya agano la pili.^h **8** Kwa maana anaona hatia ya watu anaposema: “‘Tazama! Siku zinakuja,’ asema Yehova,* ‘nitakapofanya agano jipya pamoja na nyumba ya Israeli^e wa nyumba ya Yuda. **9** Halitakuwa kama agano nililofanya pamoja na mababu zao siku niliyowashika mkono na kuwaongoza kutoka nchini Misri,ⁱ kwa sababu hawakundelea kulishika agano langu, basi nikaacha kuwajali,’ asema Yehova.*

10 “‘Kwa maana hili ndilo agano nitakalofanya pamoja na nyumba ya Israeli baada ya siku hizo,’ asema Yehova.* ‘Nitazitia sheria zangu katika akili yao, nami nitaziandika katika moyo yao.’ Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.^k

11 “‘Nao hawatafundishana tena kila mtu na raia mwen-

8:6 *Au “utumishi wa watu wote ulio bora.” 8:8-11 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 8

a Ebr 7:14

b Kol 2:16, 17
Ebr 10:1

c Ebr 9:9, 24

d Kut 25:9, 40
Kut 26:30
Hes 8:4

e 1Ti 2:5

f 1Ko 11:25
Ebr 7:22
Ebr 9:15
Ebr 12:22, 24g Zb 110:4
Ro 8:17

h Ebr 7:11, 18

i Kut 12:51

j Ro 2:29

k 2Ko 6:16

Safu ya 2

a Yer 31:31-34

b Ro 10:4
Ebr 7:12

c Kol 2:13, 14

SURA YA 9

d Kut 25:8

e Hes 4:9

f Kut 40:22-24

g Kut 26:33

h Kut 36:35

i Kut 26:31, 33

j Law 16:12
Ufu 8:3

k Kut 40:21

l Kut 25:10, 11

m Kut 16:33

n Hes 17:10

o Kut 32:15

p Kut 25:18, 22
Hes 7:89

zake na kila mtu na ndugu yake, wakisema: “Mjue Yehova!”* Kwa maana wote watanijua, kuanzia mdogo zaidi mpaka aliye mkubwa zaidi miongoni mwa. **12** Kwa maana nitaonyesha rehema kwa matendo yao yasiyo ya uadilifu, nami sitazikumbuka tena dhambi zao.”^a

13 Anaposema “agano jipya,” amelifanya lile la zamani lichakae.^b Basi kile kilichochakaa na kuzeeka kiko karibu kutoweka.^c

9 Basi, kwa upande wake, lile agano la zamani lilikuwa na matakwa ya kisheria kwa ajili ya utumishi mtakatifu na mahali pake patakatifu^d duniani. **2** Kwa maana chumba cha kwanza cha hema kilijengwa, na ndani yake mlikuwa na kinara cha taa^e na meza na mikate ya toleo;^{*f} nacho kinaitwa Mahali Patakatifu.^g **3** Lakini nyuma ya pazia la pili^h kulikuwa na chumba cha hema kilichoitwa Patakatifu Zaidi.ⁱ **4** Hicho kilikuwa na chetezo cha dhahabu/na sanduku la agano^k likiwa limefunikwa kabisa kwa dhahabu,^l ambalo ndani yake mlikuwa na mtungi wa dhahabu wenye mana,^m fimbo ya Haruni iliyochipuka,ⁿ na yale mabamba^o ya agano; **5** na juu yake palikuwa na wale makurubi wenye utukufu waliokifunika kile kifuniko cha upatanisho.^{*p} Lakini sasa si wakati wa kuzungumzia mambo hayo kirefu.

6 Baada ya vitu hivyo kujengwa kwa njia hiyo, makuhani huingia katika chumba cha kwanza cha hema kwa uka-

9:2 *Au “mikate ya wonyesho.” 9:5 *Au “mahali pa kufunika dhambi.”

waida ili kutoa utumishi mtakatifu;^a **7** lakini kuhani mkuu huingia ndani ya chumba cha pili akiwa peke yake mara moja kwa mwaka,^b akiwa na damu,^c ambayo huitoa kwa ajili yake mwenyewe^d na kwa ajili ya dhambi ambazo watu^e walifanya bila kujua. **8** Hivyo roho takatifu hufanya iwe wazi kwamba njia ya kuingia mahali patakatifu bado haikuwa imefunuliwa lile hema la zamani lilipokuwa limesimama.^f **9** Hema hili ni mfano kwa ajili ya wakati huu,^g na kulingana na mpango huu, zawadi na dhabihu zinatolewa.^h Hata hivyo, haziwezi kufanya dhamiri ya mtu anayefanya utumishi mtakatifu iwe kamilifu.ⁱ **10** Zinahuu vyakula na vinywaji tu na njia mbalimbali za kujisafisha kisherhe.^{*j} Hayo yalikuwa matakwa ya kisheria kuhusu mwili^k nayo yalifuatwa mpaka wakati uliowekwa wa kunyoosha mambo.

11 Hata hivyo, Kristo alipokuja akiwa kuhani mkuu wa mambo mema ambayo tayari yamefanyika, aliingia katika hema kubwa na kamilifu zaidi ambalo halikutengezwa kwa mikono, yaani, si la uumbaji huu. **12** Aliingia mahali patakatifu, si kwa damu ya mbuzi na ya ng'ombe dume wachanga, bali kwa damu yake mwenyewe,^l mara moja kwa wakati wote, na kupata ukombozi wa* milele kwa ajili yetu.^m **13** Kwa maana ikiwa damu ya mbuzi na ya ng'ombe dumeⁿ na majivu ya ndama jike yaliyonyunyizwa juu ya wale ambao

9:10 *Tnn., "ubatizo wa aina mbalimbali." 9:12 *Tnn., "fidia ya; wokovu wa."

SURA YA 9

a Law 24:3, 4

b Law 16:2

c Kut 30:10
Law 16:14

d Law 16:6, 11

e Law 16:15

f Ebr 10:19, 20

g Kol 2:16, 17
Ebr 8:5
Ebr 10:1

h Law 23:37, 38

i Gal 3:21
Ebr 7:11, 19

j Kut 30:17-19

k Hes 19:13

l Ebr 12:24
Ebr 13:20m Da 9:24
Mt 20:28
1Ti 2:5, 6

n Law 16:6, 15

Safu ya 2

a Hes 19:9, 17, 19

b 1Pe 1:18, 19

c 1Yo 1:7

d Ro 12:1

e Lu 22:20
1Ti 2:5
Ebr 12:22, 24

f Mt 20:28

g Ro 8:17

h Kut 24:6-8

i Kut 29:12
Law 8:15

j Law 17:11

k Law 9:7-9

wametiwa unajisi hutakasa ili kuusafisha mwili,^a **14** je, damu ya Kristo,^b ambaye kupitia roho inayodumu milele alijitoa mwenyewe kwa Mungu bila dosari, haitazisafisha hata zaidi dhamiri zetu kutoka katika matendo yaliyokufa^c ili tumtolee utumishi mtakatifu Mungu aliye hai?^d

15 Hiyo ndiyo sababu yeye ni mpatanishi wa agano jipya,^e ili kwa sababu kifo kimetokea kusudi waachiliwe huru kupitia fidia^f kutoka kwenye makosa chini ya agano la zamani, wale ambao wameitwa waipokee ahadi ya urithi unaodumu milele.^g **16** Kwa maana palipo na agano, kifo cha mwana-damu anayefanya agano kinahitaji kuthibitishwa, **17** kwa sababu agano huwa halali kifo kinapotokea, kwa kuwa halitumiki ikiwa mwanadamu anayefanya agano bado yuko hai.

18 Kwa hiyo, lile agano la zamani halikuanza kutumika* bila damu. **19** Kwa maana Musa alipowatajia watu wote kila amri ya Sheria, alichukua damu ya wale ng'ombe dume wachanga na ya wale mbuzi, pamoja na maji, sufu nyekundu, na hisopo, na kukinyunyizia kile kitabu* na watu wote, **20** akisema: "Hii ndiyo damu ya agano ambalo Mungu amewaamuru mlishi-ke."^h **21** Vilevile alilinyunyizia damu lile hema na vyombo vyote vya utumishi mtakatifu.^{*i} **22** Ndiyo, kulingana na Sheria karibu vitu vyote husafishwa kwa damu,^j na hakuna msamaha unaopatikana bila kumwaga damu.^k

9:18 *Tnn., "halikuzinduliwa." 9:19 *Au "kitabu cha kukunjwa." 9:21 *Au "utumishi wa watu wote."

23 Kwa hiyo, ilikuwa muhimu kwa mifano ya uhalisi^a wa vitu vilivyvo mbinguni kushafishwa kwa njia hiyo,^b lakini vitu vya mbinguni vinahitaji dhabihu zilizo bora zaidi.

24 Kwa maana Kristo hakuingia mahali patakatifu paliopotengenezwa kwa mikono,^c ambapo ni mfano wa uhalisi,^d bali aliingia mbinguni kwenyewe,^e hivi kwamba sasa anaonekana mbele za* Mungu kwa ajili yetu.^f 25 Hilo halikufanywa ili ajitoe mwenyewe mara nyingi, kama kuhani mkuu anavyoingia mahali patakatifu mwaka baada ya mwaka^g akiwa na damu ambayo si yake mwenyewe. 26 La sivyo, ingekuwa lazima ateseke mara nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu. Lakini sasa amejifunua mara moja kwa wakati wote kwenye umalizio wa mifumo ya mambo* ili kuondoa dhambi kupitia dhabihu yake mwenyewe.^h 27 Na kama vile watu wamewekwa akiba kufa mara moja kwa wakati wote, lakini baada ya hapo wapokee hukumu, 28 vivyo hivyo pia Kristo alitolewa mara moja kwa wakati wote ili kubeba dhambi za wengi;ⁱ na mara ya pili atakapotokea itakuwa bila dhambi,* naye ataonwa na wale wanaomtazamia kwa bidii kwa ajili ya wokovu wao.^j

10 Kwa kuwa Sheria ina kuvuli^k cha mambo mema yatakayokuja,^l lakini si uhalisi wa mambo hayo, haiwezi* kamwe kwa dhabihu zile-

9:24 *Tnn., "mbele za uso wa." 9:26 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Mfumo wa mambo." 9:28 *Au "hatakuja kushughulika na dhambi." 10:1 *Au labda, "watu hawawezi."

SURA YA 9

a Ebr 8:5
Ebr 9:9

b Law 16:19, 20

c Ebr 8:1, 2

d Kol 2:16, 17

e Ebr 6:19, 20
Ebr 9:12

f Law 16:15
Ro 8:34

g Law 16:2, 34

h Da 9:24
Ebr 7:27
1Pe 3:18

i Isa 53:12
Ro 6:10
1Pe 2:24

j 2Ti 4:8
Tit 2:13

SURA YA 10

k Ebr 8:5

l Kol 2:16, 17

Safu ya 2

a Ebr 7:19
Ebr 9:9

b Law 16:34

c Zb 40:6

d Zb 40:8

e Zb 40:6-8

f Gal 1:4

g Ebr 13:12

h 1Sa 2:27, 28

i Kut 29:38
Hes 28:3

j Ebr 7:18
Ebr 10:1

zile zinazotolewa mwaka baada ya mwaka, kuwafanya wale wanaokaribia wawe wakamili-fu.^a 2 La sivyo, je, dhabihu hazingekoma kutolewa, kwa sababu wale wanaotoa utumishi mtakatifu baada ya kusafishwa mara moja hawangehisi wana dhambi tena? 3 Kinyume chake, dhabihu hizo ni kikumbusho cha dhambi mwaka baada ya mwaka,^b 4 kwa maana damu ya ng'ombe dume na ya mbuzi haiwezi kuondoa dhambi.

5 Basi anapokuja katika ulimwengu anasema: "Hukutaka dhabihu na toleo, bali ulinitayarishia mwili. 6 Hukukubali dhabihu nzima za kuteketezwa na dhambi za dhambi."^c 7 Kisha nikasema: "Tazama! nimekuja (katika kitabu cha kukunjwa imeandikwa kunihusu) kufanya mapenzi yako, Ee Mungu."^d 8 Kwanza aliposema: "Hukutaka wala hukukubali dhabihu, matoleo, dhabihu nzima za kuteketewa, na dhambi za dhambi"—dhabihu zinazotolewa kulingana na Sheria— 9 kisha anasema: "Tazama! nimekuja kufanya mapenzi yako."^e Anaondoa la kwanza ili asimamishe la pili. 10 Kwa "mapenzi" hayo^f sisi tumetakaswa kupitia toleo la mwili wa Yesu Kristo mara moja kwa wakati wote.^g

11 Pia, kila kuhani husimama mahali pake siku kwa siku ili kutoa utumishi mtakatifu^h na kutoa mara nyingi dhabihu zilezile,ⁱ ambazo haziwezi kuondoa kabisa dhambi.^j 12 Lakini mtu huyu alitoa dhambi moja kwa ajili ya dhambi daima na kuke-

10:11 *Au "kufanya utumishi wa watu wote."

ti kwenye mkono wa kuu-me wa Mungu,^a **13** tangu wakati huo akisubiri mpaka adui zake wawekwe kuwa kiti cha miguu yake.^b **14** Kwa maana kupitia toleo moja la dhahabu amewafanya wale wanaotakaswa wawe wakamilifu^c dai-ma. **15** Zaidi ya hayo, roho takatifu pia inatutolea ushahidi, kwa maana baada ya kusema: **16** “Hili ndilo agano nitakalofanya pamoja nao baada ya siku hizo,” asema Yehova.* ‘Nitazitia sheria zangu katika mioyo yao, nami nitaziandika katika akili zao.’^d **17** Kisha inasema: “Nami sitazikumbuka tena dhambi zao na matendo yao ya kuasi sheria.”^e **18** Sasa kunapokuwa na msamaha wa mambo hayo, hakuna tena toleo kwa ajili ya dhambi.

19 Kwa hiyo, akina ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri* wa njia ya kuingia katika mahali patakatifu^f kwa damu ya Yesu, **20** aliyotufungulia* kuwa njia mpya na yenye uzima kupitia lile pazia,^g yaani, mwili wake, **21** na kwa kuwa tuna kuhanu mkuu aliye juu ya nyumba ya Mungu,^h **22** acheni tukaribie tukiwa na mioyo minyoo-fu na imani kamili, mioyo yetu ikiwa imenyunyizwa na kuwa safi kutokana na dhamiri yenye uovuⁱ na miili yetu ikiwa imeoshwa kwa maji safi.^j **23** Acheni tushike imara tangazo la hadharani la tumaini letu bila kuyumbayumba,^k kwa maana yule aliyeahidi ni mwaminifu. **24** Na acheni tufikiriane* ili kuchocheana* katika upendo na matendo ma-

10:16, 30 *Angalia Nyongeza A5. **10:19** *Au “uhakika.” **10:20** *Tnn., “ali-yotuzindulia.” **10:24** *Au “tuhangai-kiane.” *Au “kuhimizana.”

SURA YA 10

a Ro 8:34

b Zb 110:1
1Ko 15:25

c Ebr 7:19

d Yer 31:33
Ebr 8:10e Yer 31:34
Ebr 8:12

f Ebr 9:8, 24

g Mt 27:51

h Zek 6:13
Ebr 3:6

i 1Yo 1:7

j Efe 5:25, 26

k 1Ko 15:58
Kol 1:23

Safu ya 2

a Kol 3:23
1Ti 6:18b Kum 31:12
Mdo 2:42c Isa 35:3
Ro 1:11, 12d Ro 13:11
2Pe 3:11, 12

e 2Pe 2:21

f Mt 12:32
Ebr 6:4-6
1Yo 5:16

g Isa 26:11

h Kum 17:6

i Mt 26:27, 28
Lu 22:20

j Ebr 6:4-6

k Kum 32:35, 36

l 2Ko 4:6
Ebr 6:4

zuri,^a **25** bila kuacha kukuta-na pamoja,^b kama wengine walivyo na desturi, bali tutiane moyo,^c na kufanya hivyo zaidi kwa kadiri mnavyoona siku ile ikikaribia.^d

26 Kwa maana tukiendelea kutenda dhambi kimakusudi baada ya kupokea ujuzi sahihi wa kweli,^e hakuna tena dhahabu yoyote iliyobaki kwa ajili ya dhambi,^f **27** bali kuna tarajio hakika linaloogopesha la hukumu na hasira inayowaka itakayowaangamiza wale wanaopinga.^g **28** Mtu yeyote ambaye ameipuuza Sheria ya Musa hufa bila huruma, kwa ushuhuda wa watu wawili au wata-tu.^h **29** Mnafikiri mtu ambaye amemkanyagia chini Mwana wa Mungu na ambaye ameiona kuwa yenye thamani ya kawaida tu damu ya aganoⁱ ambayo kupitia hiyo alitakaswa, na ambaye ameidharau roho ya fadhili zizizostahiliwa, atapata adhabu kubwa kadiri gani?^j **30** Kwa maana tunamjua Yule aliyesema: “Kisasi ni changu; mimi nitalipa.” Na tena: “Yehova* atawahukumu watu wake.”^k **31** Ni jambo lenye kuogopesha kuanguka mikononi mwa Mungu aliye hai.

32 Hata hivyo, endeleeni kuzikumbuka siku za zamani ambazo, baada ya kupata nuru,^l mlivumilia pambano kubwa pamoja na mateso. **33** Nyakati fulani mlifunuliwa hadharani* kwa shutuma na dhiki pia, na nyakati fulani mlishiriki* pamoja na wale waliokuwa wakipatwa na mambo kama hayo. **34** Kwa maana mliwasikitikia wale waliokuwa

10:33 *Tnn., “mlifunuliwa kama katika ukumbi wa maonyesho.” *Au “mliungana.”

gerezani na pia kwa shangwe mkakubali kuporwa mali zenu,^a mkijua kwamba ninyi wenyewe mna urithi* bora na wenye kudumu.^b

35 Kwa hiyo, msikutupe ujasiri wenu,* ambao utathawabishwa sana.^c **36** Kwa kuwa mnahitaji uvumilivu,^d ili baada ya kufanya mapenzi ya Mungu, mpokee utimizo wa ile ahadi. **37** Kwa maana bado “muda kidogo sana,”^e na “yule anayekuja atafika naye hatakawia.”^f **38** “Lakini mwadilifu wangu ataishi kupitia imani,”^g naye “akirudi nyuma kwa kutemeka, mimi sipe ndezwi* naye.”^h **39** Sasa sisi si namna ya watu wanaorudi nyuma kwenye maangamizi,ⁱ bali sisi ni watu walio na imani ya kuhifadhi uhai wetu.*

11 Imani ni tarajio lililohakikishwa la mambo yanayotumainiwa,^j uthibitisho ulio wazi* wa mambo halisi ambayo hayaonekani. **2** Kwa maana kupitia imani, watu wa nyakati za kale* walitolewa ushahidi.

3 Kwa imani tunatambua kwamba mifumo ya mambo* ilipangwa kwa utaratibu kwa neno la Mungu, hivi kwamba kile kinachoonekana, kimekuwapo kutokana na vitu visivyoonekana.

4 Kwa imani, Abeli alimtolea Mungu dhabihu ya thamani kubwa zaidi kuliko ile ya Kaini,^k na kupitia imani hiyo alitolewa ushahidi kwamba aliku-

10:34 *Au “miliki.” 10:35 *Tnn., “uhuru wenu wa kusema.” 10:38 *Au “nafsi yangu haipendezwi.” 10:39 *Au “nafsi zetu.” 11:1 *Au “uthibitisho wenye kuridhisha.” 11:2 *Au “mababu zetu.” 11:3 *Au “vizazi.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 10

a Mt 5:12

b Lu 16:9

c Mt 10:32
1Ko 15:58d Lu 21:19
Yak 5:11

e Isa 26:20

f Hab 2:3
2Pe 3:9g Yoh 3:16
Ro 1:17

h Hab 2:4

i 2Pe 2:20

SURA YA 11

j Ebr 11:13

k Mwa 4:5

Safu ya 2

a Mwa 4:4

b Mwa 4:8,10

c Mwa 5:22
Yud 14

d Mwa 5:24

e Zb 58:11
Sef 2:3
Mt 5:12
Mt 6:33

f Mwa 6:8,9

g Mwa 6:13,17

h Mwa 6:14

i Mwa 6:22
2Pe 2:5

j Ro 4:9,11

k Mwa 12:1,4

l Mwa 23:4

m Mwa 12:8

n Mwa 17:6
Mwa 26:3
Mwa 28:13

o Ebr 11:16

wa mwadilifu, kwa kuwa Mungu alikubali* zawadi zake,^a na ingawa alikufa, bado anazungumza^b kupitia imani yake.

5 Kwa imani, Enoko^c alihamishwa ili asione kifo, naye hakupatikana popote kwa sababu Mungu alikuwa amemhamisha;^d kwa maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ametolewa ushahidi kwamba amempendeleza Mungu vema. **6** Isitoshe, bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu vema, kwa maana yule anayemkaribia Mungu lazima aamini kuwa yuko* na kwamba yeye huwa mthawabishaji wa wale wanaomtafuta kwa bidii.^e

7 Kwa imani, Noa^f baada ya kuonywa na Mungu kuhusu mambo ambayo bado hayakuwa yameonekana,^g alimtii Mungu* kwa kujenga safina^h kwa ajili ya kuiokoa nyumba yake; na kupitia imani hiyo alihukumu ulimwengu,ⁱ naye akawa mrithi wa uadilifu unaotokana na imani.

8 Kwa imani, Abrahamu/^j alipoitwa alitii kwa kutoka na kwenda mahali ambapo angepokea kuwa urithi; aliiondoka, ingawa hakujua mahali alipokuwa akienda.^k **9** Kwa imani aliishi akiwa mgeni katika nchi ya ahadi kama katika nchi ya kigeni,^l akiishi kwenye mahema^m pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ileile.ⁿ

10 Kwa maana alikuwa akiangojea jiji lililo na misingi ya kweli, ambalo mbuni* na mjenzi wake ni Mungu.^o

11 Kwa imani, Sara pia alipokea nguvu za kupata

11:4 *Au “alitoa ushahidi kwa kukubali.” 11:6 *Au “yuko hai.” 11:7 *Au “alimwogopa Mungu.” 11:10 *Au “msanifu.”

uzao,* ingawa alikuwa amepita umri,^a kwa kuwa alimwona kuwa mwaminifu[#] Yule aliyekuwa ameahidi. **12** Kwa sababu hiyo, kutoka kwa mwanaumume mmoja, ambaye alikuwa kama mfu,^b walizaliwa watoto^c wengi kama nyota za mbinguni na wasiohesabika kama mchanga ulio kando ya bahari.^d

13 Katika imani hawa wote walikufa, ingawa hawakupokea utimizo wa zile ahadi,^e bali waliziona kwa mbali^f na kuzikaribisha na kutangaza hadharani kwamba walikuwa wageni na wakaaji wa muda katika nchi. **14** Kwa maana wale wanaozungumza hivyo wanathibitisha kwamba wanatafuta kwa bidii mahali pao wenyewe. **15** Na bado, kama wangeendelea kukumbuka mahali walipokuwa wametoka,^g wangepata nafasi ya kurudi. **16** Lakini sasa wanajitahidi kufikia mahali bora zaidi, yaani, panapohusiana na mbinguni. Kwa hiyo, Mungu haoni aibu kuwahusu, anapoitwa Mungu wao,^h kwa maana ametayarisha jiji kwa ajili yao.ⁱ

17 Kwa imani, Abrahamu alipojaribiwa,^j ni kana kwamba alimtoa Isaka—mtu huyo aliyekuwa amezipokea ahadi kwa furaha alijaribu kumtoa mwana wake mzaliwa-pekee^k— **18** ingawa alikuwa ameambiwa: “Ule utakaoitwa uzao* wako utapitia kwa Isaka.”^l **19** Lakini alifikia uamuzi kwamba Mungu angeweza kumfufua hata kutoka kwa wafu, naye alimpokea kutoka huko kwa njia ya mfano.^m

11:11, 18 *Tnn., “mbegu.” 11:11 #Au “anayetegemeka.”

SURA YA 11

a Mwa 17:17

Mwa 21:2

b Ro 4:19

c Mwa 21:5

d Mwa 22:17

IFa 4:20

e Mwa 47:9

f Yoh 8:56

g Mwa 11:31

h Kut 3:6, 15

i Ebr 11:10

Ebr 12:22

j Mwa 22:1, 2

k Mwa 22:9, 10

Yoh 3:16

l Mwa 21:12

m IKo 10:11

Safu ya 2

a Mwa 27:27-29

b Mwa 27:38-40

c Mwa 47:29

d Mwa 48:15, 16, 20

e Mwa 47:31

f Mwa 50:24, 25

Kut 13:19

g Kut 2:2

h Mdo 7:20

i Kut 1:16, 22

j Kut 2:11

k Kut 2:10

l Kut 12:51

m Kut 10:28

n ITi 1:17

o Kut 12:21-23

p Kut 14:22

q Kut 14:27, 28

20 Kwa imani pia, Isaka alimbariki Yakobo^a na Esau^b kuhusu mambo yatakayokuja.

21 Kwa imani, Yakobo alipokuwa karibu kufa,^c aliwabariki wana wawili wa Yosefu^d na akaabudu huku akiegemea juu ya fimbo yake.^e

22 Kwa imani, Yosefu aki-karibia mwisho wake, alizungumza kuhusu kutoka* kwa wana wa Israeli, naye akawapa maagizo[#] kuhusu mifupa^Δ yake.^f

23 Kwa imani, Musa alifichwa kwa miezi mitatu na wazazi wake baada ya kuzaliwa,^g kwa sababu waliona kwamba huyo mtoto mchanga alikuwa mwenye kupendeza^h nao hawakuliogopa agizo la mfalme.ⁱ **24** Kwa imani, Musa alipokuwa mtu mzima,^j alikataa kuitwa mwana wa binti ya Farao,^k **25** akachagua kuteswa pamoja na watu wa Mungu badala ya kufurahia dhambi kwa muda, **26** kwa sababu aliona shutuma ya Kristo kuwa utajiri mkubwa kuliko hazina za Misri, kwa maana alikaza macho kwenye malipo ya thawabu. **27** Kwa imani aliondoka Misri,^l lakini hakuogopa hasira ya mfalme,^m kwa maana aliendelea kuwa imara kama mtu anayemwona Yule asiyeonekana.ⁿ **28** Kwa imani alifanya sherehe ya Pasa-ka na kupaka damu, ili mwangamizaji asiwadhuru* wazaliwa wao wa kwanza.^o

29 Kwa imani walipita katika Bahari Nyekundu kama kwenye nchi kavu,^p lakini Wamisri walipojaribu kupita wakamezwa.^q

11:22 *Yaani, kutoka katika nchi ya Misri. #Au “amri.” ΔAu “mazishi.” 11:28 *Tnn., “asiwaguse.”

30 Kwa imani kuta za Yeri-ko zilianguka baada ya watu kuzizunguka kwa siku saba.^a

31 Kwa imani, Rahabu yule kahaba hakuangamia pamoja na wale waliokosa kutii, kwa sababu aliwapokea wale wa-pelelezi kwa amani.^b

32 Nami nitasema nini zaidi? Kwa maana nitakosa wakati nikiendelea kusimulia kuhusu Gideoni,^c Baraka,^d Samsoni,^e Yeftha,^f Daudi,^g na vilevile Samweli^h na wale manabii wengine. **33** Kupitia imani walishinda falme,ⁱ wakaleta uadilifu, wakapata ahadi,^j wakaziba vinywa vya simba,^k

34 wakazima nguvu za moto,^l wakaponyoka makali ya upanga,^m wakafanywa kuwa wenyewe nguvu kutoka kwenye hali ya udhaifu,ⁿ wakawa mashujaa katika vita,^o wakayashinda kabisa majeshi ya wavamizi.^p **35** Wanawake waliwapokea wafu wao kupitia ufufuo,^q lakini watu wengine waliteswa kwa sababu hawakukubali kuachiliwa kupitia fidia fulani, ili waupate ufufuo ulio bora. **36** Ndiyo, wengine walipata jaribu lao kwa kudhihakiwa na kupigwa kwa mijeledi, naam, isitoshe, kwa kufungwa minyororo^r na magerezani.^s **37** Walipigwa mawe,^t walijaribiwa, walikatwa vipande viwili* kwa msumeno, walichinjwa kwa upanga,^u walitembea huku na huku wakiwa wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi,^v wakiwa katika uhitaji, katika dhiki,^w wakiteswa;^x **38** na ulimwengu haukuwafaa. Walitembea huku na huku katika majangwa na milima na mapango^y na mashimo ya dunia.

11:37 *Au "vipandevipande."

SURA YA 11

a Yos 6:15, 20

b Yos 6:17

c Amu 6:11

d Amu 4:6

e Amu 13:24

f Amu 11:1

g 1Sa 16:13

h 1Sa 3:20

i Amu 7:12, 22

j 2Sa 7:8, 12

k Amu 14:5, 6

1Sa 17:34-36

Da 6:21, 22

l Da 3:23-25

m 2Fa 6:15, 16

n Amu 16:28

1Fa 18:46

o Amu 11:32

p Amu 4:16

q 1Fa 17:22-24

2Fa 4:32, 34

r Yer 20:2

s Yer 37:15

t 2Nya 24:20, 21

u 1Fa 19:10

v 2Fa 1:8

w 1Fa 19:2

x 1Fa 22:24

Yer 38:6

y 1Fa 18:4

1Fa 19:9

Safu ya 2

a Ebr 2:3

Ebr 3:1

Ebr 7:22

SURA YA 12

b Ebr 3:12

c 1Ko 9:24, 26

Flp 3:13, 14

d Yoh 14:6

Mdo 5:31

Ebr 2:10

e Zb 110:1

Ebr 10:12

f Mt 27:39

g Gal 6:9

h Met 3:11, 12

39 Na bado hawa wote, ingawa walitolewa ushahidi unaofaa kwa sababu ya imani yao, hawakupata utimizo wa ile ahadi, **40** kwa sababu Mungu aliona mapema kitu bora kwa ajili yetu,^a ili wasifanywe kuwa wakamilifu bila sisi.

12 Hivyo basi, kwa kuwa tuna wingu kubwa hivyo la mashahidi linalotuzunguka, acheni sisi pia tuondoe kila uzito na dhambi inayotutatanisha kwa urahisi,^b na tukimbie kwa uvumilivu shindano la mbio lililolekwa mbele yetu,^c **2** huku tukimtazama kwa makini Wakili Mkuu na Mkamilishaji wa imani yetu, Yesu.^d Kwa sababu ya shangwe iliyowekwa mbele yake, alivumilia mti wa mateso,^e akaidharau aibu, naye ameketi kwenye mkono wa kuume wa kiti cha ufalme cha Mungu.^e **3** Kwa kweli, mfikirieni sana yule ambaye amevumilia maneno makali kama hayo kutoka kwa watenda dhambi^f kinyume cha faida zao wenyewe, ili msichoke na kukata tamaa.^{*g}

4 Katika pambano lenu na dhambi, hamjapambana kamwe kufikia hatua ya kumwaga damu. **5** Nanyi mmesahau kabisa lile himizo linalosema nanyi kama wana: "Mwanangu, usiipuuzo nidhamu kutoka kwa Yehova,^{*} wala usikate tamaa anapokurekebisha; **6** kwa maana Yehova^{*} huwatia nidhamu wale anawapenda, kwa kweli, humpiga fimbo[#] kila mtu ambaye amepokea kuwa mwana."^h

12:2 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 12:3 *Au "msizimie katika nafsi zenu." 12:5, 6 *Angalia Nyongeza A5. 12:6 #Au "humwadhibu."

7 Mnahitaji kuvumilia kama sehemu ya nidhamu* yenu. Mungu anawatendea ninyi kama wana.^a Kwa maana ni mwana gani ambaye hatiwi nidhamu na baba yake?^b **8** Lakini ikiwa ninyi nyote hamjashiriki katika kupokea nidhamu hii, kwa kweli ninyi ni watoto haramu, bali si wana. **9** Zaidi ya hayo, baba zetu wa kibinadamu* walikuwa wakitulia nidhamu, nasi tuliwapa heshima. Je, hatupaswi kujiitiisha hata zaidi kwa Baba wa maisha yetu ya kiroho na kuishi?^c **10** Kwa maana walitulia nidhamu kwa muda mfuupi kulingana na jinsi walivyoona kuwa inafaa, lakini yeye hufanya hivyo kwa faida yetu ili tuushiriki utakatifu wake.^d **11** Ni kweli, hakuna nidhamu inayoonekana kwa sasa kuwa yenye shangwe, bali inaumi-za;* lakini baadaye hutokeza amani na uadilifu^e kwa wale ambao wamezoezwa nayo.

12 Kwa hiyo, imarisheni mikonu inayolegea na magoti yaliyo dhaifu,^e **13** nanyi endeleeni kuifanyia miguu yenu mapito yaliyonyooka,^f ili kile ambacho ni kilemavu kisiteguke, badala yake, kiponywe. **14** Fuatilieni amani pamoja na watu wote^g na utakaso*^h ambao bila huo hakuna mtu atakayemwona Bwana. **15** Iweni waangalifu kwamba yeyote asikoe kupata fadhili zizizostahiliwa za Mungu, ili mzizi wowote wenye sumu usichipuke na kusababisha taabu na wengi watiwe unajisi

12:7 *Au "mazoezi." 12:9 *Tnn., "baba zetu wa mwili." 12:11 *Au "inahuzunisha." #Tnn., "huzaa tunda lenye kufanya amani la uadilifu." 12:14 *Au "utakatifu."

SURA YA 12

a 2Sa 7:14
Ebr 2:10

b Met 13:24

c Yak 4:10

d 1Pe 1:15, 16

e Isa 35:3

f Met 4:26

g Zb 34:14
Ro 12:18
Ro 14:19

h Ro 6:19
1Th 4:3, 4
Ebr 10:10

Safu ya 2

a Kum 29:18

b Mwa 25:32, 34

c Mwa 27:34

d Kut 19:12

e Kut 19:18

f Kut 19:16

g Kut 19:19

h Kum 4:11, 12

i Kut 20:18, 19

j Kut 19:12, 13

k Kum 9:19

l Ufu 14:1

m Ufu 21:2

n Da 7:10

o Mwa 18:25
Zb 94:2
Isa 33:22

p Ebr 12:9

q Ebr 10:14

r 1Ti 2:5
Ebr 9:15

s Mt 26:27, 28

t Mwa 4:8, 10

nao;^a **16** na muwe waangalifu ili miongoni mwenu kusiwe na mwasherati* wala yeyote asiyethamini mambo matakatifu, kama Esau, aliyetoa haki zake za kuwa mzaliwa wa kwanza kwa kubadilishana na mlo mmoja.^b **17** Kwa kuwa mnajua kwamba baadaye alipotaka kuirithi baraka, alikataliwa; kwa maana, ingawa alijaribu kwa bidii kubadili fikira* kwa machozi,^c hakufaulu.[#]

18 Kwa maana hamkukaribia kitu kinachoweza kuguswa^d na ambacho kimewashwa moto,^e na wingu jeusi na giza zito na dhoruba,^f **19** na mlio wa tarumbeta^g na sauti ya maneno yanayosemwa,^h ambayo watu walipoisikia waliomba kwamba wasiambiwe neno lingine lolote.ⁱ **20** Kwa maana hawakuweza kuivumilia amri hii: "Hata mnyama akiugusa mlima, lazima apigwe mawe."^j **21** Pia, wonyesho huo ulikuwa wa kutisha sana hivi kwaomba Musa akasema: "Ninaogopa na kutetemeka."^k **22** Lakini ninyi mmeukaribia Mlima Sayuni,^l jiji la Mungu aliye hai, yaani, Yerusalemu la mbinguni,^m na makumi ya maelfu ya malaika **23** katika kusanyiko kuu,ⁿ na kutaniko la wazaliwa wa kwanza ambao wameandikishwa mbinguni, na Mungu Mwamuzi wa wote,^o na maisha ya kiroho^p ya waadilifu ambao wamefanya wakamilifu,^q **24** na Yesu mpananishi^r wa agano jipya,^s na damu iliyonyunyizwa, ambayo husema kwa njia bora kuliko damu ya Abeli.^t

12:16 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Uasherati." 12:17 *Yaani, fikira za baba yake. #Tnn., "hakupata nafasi kwa ajili ya hilo."

25 Angalieni kwamba msikatae kumsikiliza* yule anayezungumza. Kwa maana ikiwa wale waliokataa kumsikiliza yule aliyetoa onyo kutoka kwa Mungu duniani hawakuponyoka, je, kweli sisi tutaponyoka ikiwa tutamwacha yule anayezungumza kutoka mbinguni?^a 26 Wakati huo sauti yake iliitikisa dunia,^b lakini sasa ameahidi: "Nitatikisa kwa mara nyingine tena, si dunia tu bali pia mbingu."^c 27 Sasa maneno "kwa mara nyingine tena" yanaonyesha kuondolewa kwa vitu vinavyotikiswa, vitu vilivyotengenezwa, ili vitu ambavyo havitikiswi vibaki. 28 Kwa hiyo, kwa kuwa tutapokea Ufalme usioweza kutikiswa, acheni tuzendelee kupokea fadhili zizozostahiliwa, ambazo zitatuwezesha kumtolea Mungu utumishi mtakatifu kwa njia inayokubalika, kwa kumwogopa Mungu na kumheshimu. 29 Kwa maana Mungu wetu ni moto unaoteketeza.^d

13 Upendo wenu wa kindugu na uendeleo.^e 2 Msisahau kuwakaribisha wageni,^f kwa maana kwa kufanya hivyo watu fulani bila kujua waliwakaribisha malaika.^g 3 Wakumbukeni wale walio gerezani,^h kana kwamba mmefungwa pamoja nao,ⁱ na wale wanaoteswa, kwa kuwa ninyi pia mko katika mwili.^h 4 Ndoa na iheshimiwe kati ya wote, na kitanda cha ndoa kisiwe na unajisi,^j

12:25 *Au "msimpe visingizio: msimpuuze." 13:2 *Au "kuwaonyesha wageni fadhili; kuwa wakarimu." 13:3 *Tnn., "waliofungwa; walio katika vifungo." ^aAu labda, "kana kwamba mnateseka pamoja nao."

SURA YA 12

a Ebr 1:2
Ebr 2:2-4

b Kut 19:18

c Hag 2:6

d Kum 4:24

SURA YA 13

e 1Th 4:9
1Pe 1:22

f Ro 12:13
1Ti 3:2

g Mwa 18:2, 3
Mwa 19:1-3

h Kol 4:18

i Ro 12:15

j Met 5:16, 20
Mt 5:28

Safu ya 2

a Met 6:32
1Ko 6:9, 10
1Ko 6:18
Gal 5:19, 21

b 1Ti 6:10

c Met 30:8, 9
1Ti 6:8

d Kum 31:6, 8

e Zb 118:6
Da 3:17
Lu 12:4

f 1Ti 5:17
Ebr 13:17

g 1Ko 11:1
2Th 3:7

h Ro 14:17
1Ko 8:8
Kol 2:16

i 1Ko 9:13
1Ko 10:18

j Law 16:27

k Yoh 19:17

l Ebr 9:13, 14

m Ro 15:3
2Ko 12:10
1Pe 4:14

n Ebr 11:10
Ebr 12:22

kwa maana Mungu atawahukumu waasherati* na wazinzi.^a 5 Njia yenu ya maisha iwe bila upendo wa pesa,^b huku mkiridhika na vitu mlivyo navyo.*^c Kwa maana amesema: "Sita kuacha wala kukutupa kamwe."^d 6 Ili tuwe hodari na kusema: "Yehova* ni msaidizi wangu; sitaogopa. Mwanadamu atanifanya nini?"^e

7 Wakumbukeni wale wanaoongoza kati yenu,^f ambao wamelisema neno la Mungu kwenu, nanyi mnapotafakari matokeo ya mwenendo wao, igeni imani yao.^g

8 Yesu Kristo ni yuleyule jana, leo, na milele.

9 Msipotoshwe na mafundi-sho mbalimbali yaliyo mage-ni, kwa maana ni bora moyo uimarishwe kwa fadhili zisizostahiliwa, bali si kwa vyakula,* ambavyo haviwanufaishi wale wanaojishughulisha navyo.^h

10 Sisi tuna madhabahu ambayo wale wanaofanya utumishi mtakatifu katika hema hawana mamlaka ya kula kilicho juu yake.ⁱ 11 Kwa maana miili ya wanyama ambao kuhani mkuu hupeleka damu yao ndani ya mahali patakatifu kama tolea la dhambi hutekelezwa nje ya kambi.^j 12 Kwa hiyo, Yesu pia aliteseka nje ya lango la jiji^k ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe.^l 13 Basi, acheni twende kwake nje ya kambi, tukiibeba shutumaliyoibeba,^m 14 kwa maana hapa hatuna jiji linalodumu, bali tunatafuta kwa bidii lile litakalokuja.ⁿ 15 Kupitia yeye sikuzote na tumtolee Mu-

13:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Uasherati." 13:5 *Au "vya sasa." 13:6 *Angalia Nyongeza A5. 13:9 *Yaani, sheria zinazohusu chakula.

ngu dhabihu ya sifa,^a yaani, tunda la midomo yetu^b ambalo hulitangaza jina lake hadhara-ni.^c **16** Zaidi ya hayo, msisahau kutenda mema na kushirikiki vitu vyenu pamoja na wengine,^d kwa maana Mungu hupendezwa na dhabihu kama hizo.^e

17 Watiini wale wanaoongoza kati yenu^f na mnyenyekee,^g kwa maana wanaandelea kuwalinda ninyi* kama wale watakaotoa hesabu,^h ili wafanye hivyo kwa shangwe na si kwa huzuni, kwa maana kufanya hivyo kungewadhuru ninyi.

18 Endeleei kusali kwa ajili yetu, kwa maana tuna hakika kwamba tuna dhamiri nyoofu,* kwa kuwa tunataka kujiendesha kwa unyoofu katika mambo yote.ⁱ **19** Lakini hasa ninawahimiza ninyi msali kwamba nirudi kwenu haraka iwezekanavyo.

13:17 *Au "kuzilinda nafsi zenu." **13:18** *Tnn., "njema."

SURA YA 13

a Law 7:12
Zb 50:14, 23

b Zb 69:30, 31
Ho 14:2

c Ro 10:9

d Ro 12:13

e Flp 4:18

f 1Th 5:12

g Efe 5:21
1Pe 5:5

h Mdo 20:28

i 2Ko 1:12

Safu ya 2

a 1Pe 5:4

b Mdo 27:1

20 Basi Mungu wa amani, aliyemrudisha kutoka kwa wafu mchungaji mkuu^a wa kondoo, Bwana wetu Yesu, kwa damu ya agano linalodumu milele, **21** awape vifaa vyote vyema ili mfanje mapenzi yake, akitenda ndani yetu kupitia Yesu Kristo mambo yanayopendeza machoni pake, na awe na utukufu milele na milele. Amina.

22 Sasa ninawahimiza, aki-na ndugu, nisikilize kwa subira neno hili la kutia moyo, kwa maana nimewaandikia barua fupi. **23** Ningependa kuwajulisha kwamba ndugu yetu Timotheo ameachiwa huru. Akija hivi karibuni, nitakuja pamoja naye kuwaona.

24 Wapeni salamu zangu wote wanaoongoza kati yenu na watakatifu wote. Wale walio Italia^b wanawatumia salamu zao.

25 Fadhili zisizostahiliwa na ziwe pamoja nanyi nyote.

BARUA YA

YAKOBO

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Salamu (1)
Uvumilivu huleta furaha (2-15)
Sifa iliyojaribiwa ya imani (3)
Endelea kuomba ukiwa na imani (5-8)
Tamaa huongoza kwenye dhambi na kifo (14, 15)
Kila zawadi njema hutoka juu (16-18)
Kusikia na kutenda neno (19-25)
Mtu anayejitazama kwenye kioo (23, 24)
Ibada safi na isiyo na unajisi (26, 27)</p> | <p>2 Upendeleo ni dhambi (1-13)
Upendo, sheria ya kifalme (8)
Imani bila matendo imekufa (14-26)
Roho waovu wanaamini na kutetemeka (19)
Abrahamu alitwa rafiki ya Yehova (23)</p> <p>3 Kuufuga ulimi (1-12)
Wengi hawapaswi kuwa walimu (1)
Hekima kutoka juu (13-18)</p> |
|--|--|

- 4 Usiwe rafiki ya ulimwengu (1-12)
Mpingeni Ibilisi (7)
Mkaribieni Mungu (8)
Onyo dhidi ya kiburi (13-17)
“Yehova akipenda” (15)
- 5 Onyo kwa matajiri (1-6)

Mungu huwabariki wanaovumilia
kwa subira (7-11)
Acheni “ndiyo” yenu iwe ndiyo (12)
Sala ya imani ina nguvu (13-18)
Kumsaidia mtenda dhambi
arudi (19, 20)

1 Yakobo,^a mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo, kwa yale makabila 12 yaliyotawanyika sehemu mbalimbali:

Salamu!

2 Oneni yote kuwa shangwe, ndugu zangu, mnapopata majaribu mbalimbali,^b **3** mkijua kwamba sifa iliyojaribiwa ya imani yenu hutokeza uvumilivu.^c **4** Lakini acheni uvumilivu ukamilishe kazi yake, ili muwe kamili na timamu katika mambo yote, bila kukosa kitu chochote.^d

5 Kwa hiyo, ikiwa yeyote kati yenu anakosa hekima, na aendelee kumwomba Mungu,^e kwa maana yeye huwapa wote kwa ukarimu na bila kushutumu,^f naye atapewa.^g **6** Lakini na aendelee kuomba kwa imani,^h bila kuwa na shaka hata kidogo,ⁱ kwa maana aliye na shaka ni kama wimbi la bahari linaloendeshwa na upepo na kupeperushwa huku na huku. **7** Kwa kweli, mtu huyo asitarajie kupokea kitu chochote kutoka kwa Yehova;^{*} **8** yeye ni mtu anayesitasita,^j asiye imara katika njia zake zote.

9 Lakini ndugu wa hali ya chini na ashangilie katika*

1:5 *Au “bila kutafuta makosa.” 1:7, 12 *Angalia Nyongeza A5. 1:9 *Tnn., “ajivunie.”

SURA YA 1

a Mt 13:55

b Mt 5:11,12

c 1Pe 1:6, 7

d 1Ko 14:20
Efe 4:13

e 1Fa 3:9
Mk 11:24
1Yo 3:22

f Mt 7:11

g Met 2:3-6
Yoh 15:7
1Yo 5:14

h Mt 7:7

i Mt 21:22
Ebr 11:6

j Yak 4:8

Safu ya 2

a Yak 2:5

b 1Ti 6:17

c Isa 40:6, 7
Mt 19:24

d Mt 5:10
Yak 1:2

e 2Ti 4:8
1Pe 5:4
Ufu 2:10

f Yak 2:5

g Mwa 3:6
1Yo 2:16

h Ro 5:21

i Mt 7:11

kuinuliwa kwake,^a **10** naye tajiri katika kushushwa kwake,^b kwa sababu atapitilia mbali kama ua la shambani. **11** Kwa maana kama jua lina-nyochochoza pamoja na joto lake linalounguzwa na kufanya mmea unyauke, na ua lake lianguke na kuharibu urembo wake wa nje, vivyo hivyo pia, tajiri atanyauka katika mambo anayofuatilia.^c

12 Mwenye furaha ni yule anayeendelea kuvumilia jaribu,^d kwa sababu atakapokubaliwa atapokea taji la uzima,^e ambalo Yehova* ali-waahidi wale wanaoendelea kumpenda.^f **13** Mtu akiwa chini ya jaribu, asiseme: “Mungu ananijaribu.” Kwa maana Mungu hawezi kujaribiwa na mambo maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu yeyote. **14** Lakini kila mtu hujaribiwa kwa kuvutwa na kushawishiwa* na tamaa yake mwenyewe.^g **15** Kisha tamaa, wakati imetunga mimba, huzaa dhambi; nayo dhambi, baada ya kufanywa, huleta kifo.^h

16 Msipotoshwe, ndugu zangu wapendwa. **17** Kila zawadi njema na kila tuzo kamilifu hutoka juu,ⁱ hushuka kutoka kwa Baba wa mianga ya

1:14 *Au “ kunaswa kama kwa kutumia chambo.”

mbinguni,^a ambaye habadiliki au kugeuka kama kivuli.*^b **18** Yalikuwa mapenzi yake kutuzaa sisi kwa neno la kweli,^c ili kwa njia fulani tuwe matunda ya kwanza ya viumbe wake.^d

19 Jueni hili, ndugu zangu wapendwa: Kila mtu lazima awe mwepesi wa kusikia, si mwepesi wa kusema,^e si mwepesi wa hasira,^f **20** kwa maana hasira ya mwanadamu haitokezi uadilifu wa Mungu.^g **21** Kwa hiyo, ondoeni uchafu wote na ubaya wote,^h na pokeeni kwa upole kupandwa kwa lile neno linaloweza kuwaokoa.[#]

22 Hata hivyo, iweni watekdaji wa neno,ⁱ na si wasikiaji tu, mkijidanganya wenye kwa mawazo ya uwongo. **23** Kwa maana ikiwa yeyote ni msikiaji wa neno, na si mtendaji,^j huyo ni kama mtu anayetazama uso wake* katika kioo. **24** Kwa maana yeye hujitazama na kwenda zake na kusahau mara moja jinsi alivyo. **25** Lakini anayechunguza sheria kamilifu^k ambayo ni ya uhuru na kudumu katika hiyo, amekuwa, si msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi; naye atafurahia kile anachofanya.^l

26 Ikiwa mtu yeyote anafiki yeye ni mwabudu wa Mungu* lakini haudhibiti[#] kabisa ulimi wake,^m anaudanganya moyo wake, na ibada yake ni ubatili. **27** Namna ya ibada* iliyo safi na isiyo na una-

1:17 *Au "ambaye habadiliki kama kugeuka kwa kivuli." 1:21 *Au labda, "wingi wa ubaya." #Au "kuokoa nafsi zenu." 1:23 *Au "uso wake wa asili." 1:26 *Au "ni mtu wa dini." #Au "hauongozi kwa kijamu." 1:27 *Au "dini."

SURA YA 1

- a Yer 31:35
2Ko 4:6
b Mal 3:6
c Yoh 1:12,13
Ro 8:28
Efe 1:13,14
2Th 2:13
1Pe 1:23
d Ufu 14:4
e Met 10:19
Met 17:27
f Mhu 7:9
Mt 5:22
g Yak 3:18
h Kol 3:8
1Pe 2:1
i Law 18:5
1Sa 15:22
Mt 7:21
1Yo 3:7
j Lu 6:46
Yak 2:14
k Zb 19:7
l Mt 7:24
Lu 11:28
Yoh 13:17
m Zb 39:1
Met 12:18
Met 15:2
1Pe 3:10

Safu ya 2

- a Kum 14:29
Kum 27:19
Zb 68:5
b Isa 1:17
1Ti 5:3
c Ayu 29:12,13
Isa 58:7
d 1Ko 5:7
Yak 4:4
Ufu 18:4

SURA YA 2

- e 1Ti 5:21
Yak 3:17
f Law 19:15
g Gal 3:28
h Kum 1:17
i Ufu 2:9
j Lu 22:28-30
k Mdo 13:50
l Law 19:18
Mt 22:39
Ro 13:10
m Yak 2:1

jisi kwa maoni ya Mungu wetu na Baba ni hii: kuwatumza mayatima^a na wajane^b katika dhiki yao,^c na kuendelea kujitunza bila doa kutokana na ulimwengu.^d

2 Ndugu zangu, je, mnashika imani ya Bwana wetu mtukufu Yesu Kristo huku mkiwa na upendeleo?^e **2** Kwa maana, ikiwa mtu aliyevaa pete za dhahabu kwenye vidole vya-ke na aliyevaa mavazi ya kifahari anaingia katika mkutano wenu, na mtu maskini aliyevaa mavazi yenye uchafu anaingia pia, **3** je, mnamtazama kwa kibali yule aliyevaa mavazi ya kifahari na kumwambia: "Wewe kalia kiti hiki kilicho mahali pazuri," na kumwambia yule maskini: "Wewe simama tu," au, "Kalia kile kiti pale chini ya kiti changu cha miguu?"^f **4** Ikiwa ndivyo ilivyo, je, hamna tofauti za kitabaka kati yenu wenyewe^g na je, hamjawa waamuzi wanaotoa maamuzi maovu?^h

5 Sikilizeni, ndugu zangu wapendwa. Je, Mungu hakuwachagua walio maskini kwa maoni ya ulimwengu ili wawe matajiri katika imaniⁱ na warithi wa Ufalme, aliowaahidi wale wanaompenda?^j **6** Lakini ninyi mmemvunja heshima maskini. Je, si matajiri wanaowakandamiza ninyi^k na kuwakokota wakiwapeleka mahakamani? **7** Je, hawalikufuru lile jina zuri ambalo kwa hilo mliitwa? **8** Basi, ikiwa mnaifuata ile sheria ya kifalme kulingana na andiko, "Lazima umpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe,"^l mnafanya vema. **9** Lakini mkiendelea kuonyesha upendeleo,^m mnafanya

dhambi, na sheria inawahukumu* kuwa wakosaji.^a

10 Kwa maana ikiwa yeyote anatii Sheria yote lakini anajikwaa katika jambo moja, amekosa kuitii Sheria yote.^b

11 Kwa maana yule aliyeseema, "Usifanye uzinzi,"^c alisema pia: "Usiue."^d Basi, ikiwa hufanyi uzinzi lakini unaua, umeivunja sheria. **12** Endelee ni kusema na kutenda kama wale watakaohukumiwa kwa sheria ya watu huru.*^e

13 Kwa maana yule asiye na mazoea ya kuonyesha rehema atahukumiwa bila rehema.^f Rehema hushinda hukumu.

14 Kuna faida gani, ndugu zangu, mtu fulani akisema ana imani lakini hana matendo?^g Je, imani hiyo inaweza kumwoko?^h **15** Ikiwa ndugu au dada hawana nguo* na chakula cha kutosha kwa ajili ya siku, **16** na mmoja wenu awaambie, "Nendeni kwa amani; mwote moto na mle vizuri," lakini bila kuwapatia mahitaji ya mwili wao, kuna faida gani?ⁱ **17** Vivyo hivyo pia, imani bila matendo imekufa.^j

18 Hata hivyo, mtu fulani atasema: "Wewe una imani, nami nina matendo. Nionyeshe imani yako bila matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa matendo yangu."^k

19 Wewe unaamini kuna Mungu mmoja, sivyo? Unafanya vema. Hata hivyo, roho wauvu pia wanaamini na kutetemeka.^k **20** Lakini je, unataka kujua, ewe mwanadamu usiye na akili, kwamba imani bila matendo haifai kitu? **21** Je, Abrahamu baba yetu haku-

SURA YA 2

a Law 19:15

b Kum 27:26
Gal 3:10c Kut 20:14
Kum 5:18d Kut 20:13
Kum 5:17

e Yak 1:25

f Met 21:13
Mt 5:7
Mt 6:15
Lu 6:36g Tit 3:8
Yak 1:25

h 1Ko 13:2

i Kum 15:7, 8
Mt 25:35, 36
Lu 3:11
Ro 12:13
1Ti 5:4
Yak 1:27
1Yo 3:17j Mt 7:21
Ebr 10:24k Mt 8:28, 29
Lu 4:33, 34

Safu ya 2

a Mwa 22:9, 12

b Ebr 11:17

c Mwa 15:6
Ro 4:3
Gal 3:6d 2Nya 20:7
Isa 41:8e Yos 2:1, 15
Yos 6:17
Ebr 11:31

f Zb 146:4

g Ro 10:10
Yak 2:17

SURA YA 3

h Lu 12:48

i 1Fa 8:46
Met 20:9
1Yo 1:8

tangazwa kuwa mwadilifu kwa matendo baada ya kumtoa Isaka mwana wake juu ya madhabahu?^a **22** Mnaona kwamba imani yake ilitenda pamoja na matendo yake na imani yake ilikamilishwa kwa matendo yake,^b **23** na andiko likatimizwa linalosema: "Abrahamu alikuwa na imani katika Yehova,* na ikahasabiwa kwake kuwa uadilifu,"^c naye akaitwa rafiki ya Yehova.*^d

24 Mnaona kwamba mtu hutangazwa kuwa mwadilifu kwa matendo, na si kwa imani peke yake. **25** Vivyo hivyo, je, Rahabu yule kahaba hakutangazwa pia kuwa mwadilifu kwa matendo, baada ya kuwakaribisha wale wajumbe na kuwatoa nje kupitia njia nyingine?^e **26** Kwa kweli, kama vile mwili bila roho* umekufa,^f vivyo hivyo, imani bila matendo imekufa.^g

3 Ndugu zangu, si wengi kati yenu wanaopaswa kuwa walimu mkijua kwamba tuta-pokea hukumu nzito* zaidi.^h

2 Kwa maana sisi sote huji-kwaa* mara nyingi.ⁱ Ikiwa yeyote hajikwai katika neno, huyo ni mtu mkamilifu, anayeweza kuongoza kwa lijamu mwili wake wote pia. **3** Tunapoweka lijamu katika vinywa vya farasi ili watutii, sisi huuongoza mwili wao wote pia. **4** Tazameni hata meli: Ingawa ni kubwa sana nazo huendeshwa na upepo mkali, zinaongozwa na mta-mbo wa usukani ulio mdogo sana ili kwenda popote ambapo mtu aliye kwenye usukani anataka.

2:23 *Angalia Nyongeza A5. 2:26 *Au "pumzi." 3:1 *Au "kali." 3:2 *Au "hufanya makosa."

2:9 *Au "inawakaripia." 2:12 *Tnn., "sheria ya uhuru." 2:15 *Tnn., "wako uchi."

5 Vivyo hivyo pia, ulimi ni kiungo kidogo cha mwili na bado hujigamba sana. Tazameni jinsi moto mdogo unavyoweza kutekeleza msitu mkubwa! 6 Ulimi pia ni moto.^a Kati ya viungo vya mwili wetu, ulimi unawakilisha ulimwengu wa ukosefu wa uadilifu, kwa maana unautia mwili wote^b najisi na kuwasha moto maisha yote* nao huwashwa moto na Gehe-na.[#] 7 Kwa maana kila aina ya mnyama wa mwituni, ndege, mnyama anayetambaa, na kiumbe wa baharini anaweza kufugwa na wamefugwa na wanadamu. 8 Lakini hakuna mwanadamu anayeweza kuufuga ulimi. Ulimi ni kitu kitundu chenye kudhuru, kili-lichojaa sumu yenye kuua.^c 9 Kwa ulimi tunamsifu Yehova,* aliye Baba, na bado kwa ulimi tunawalaani wanadamu ambao wameumbwa "kwa mfano wa Mungu."^d 10 Baraka na laana hutoka katika kinywa kilekile.

Ndugu zangu, haifai mambo yatendeke hivyo.^e 11 Je, chemchemi inaweza kutoa katika shimo lilelile maji matamu* na pia machungu? 12 Ndugu zangu, je, mtini unaweza kuzaa zeituni au mzabibu kuzaa tini?^f Maji ya chumvi hayawezi kutokeza maji matamu.*

13 Ni nani mwenye hekima na uelewaji kati yenu? Na aonyeshe kwa mwenendo wake mzuri matendo yanayofanywa kwa upole unaotokana na hekima. 14 Lakini iki-

3:6 *Tnn., "mzunguko wa uhai (chanzo)." #Angalia Kamusi, uku. 2012. 3:9 *Angalia Nyongeza A5. 3:11, 12 *Au "yasiyo na chumvi."

SURA YA 3

- a Met 16:27
Mt 12:36, 37
- b Zb 39:1
Mt 15:11, 18
Mk 7:23
- c Zb 140:3
Met 12:18
Met 18:7
- d Mwa 1:26, 27
- e Efe 4:29
- f Mt 7:16

Safu ya 2

- a Ro 13:13
1Ko 3:3
- b Efe 4:31
- c 1Ko 13:4
- d 1Ko 2:14
Flp 3:19
- e Met 14:30
Gal 5:19-21
- f Ro 12:9
1Ti 5:1, 2
- g 2Ko 13:11
1Th 5:13
2Pe 3:14
- h 1Ti 3:3
Tit 3:2
- i Gal 5:22, 23
- j Yak 2:9
- k 1Pe 1:22
- l Isa 32:17
Ebr 12:11
- m Mt 5:9
1Pe 3:11

SURA YA 4

- n Ro 7:23
Gal 5:17
Yak 3:14
1Pe 2:11
- o Mt 5:22
Yak 3:16
- p 2Nya 19:2
Yoh 15:19
Yoh 17:14
Yoh 18:36
1Yo 2:15
1Yo 5:19

wa mna wivu mkali^a na ugomvi^{*b} mioyoni mwenu, msiwe mkijigamba^c na kusema uwongo kuhusu ile kweli. 15 Hii siyo hekima inayoshuka kutoa juu; bali ni ya kidunia,^d ya kinyama, na ya roho waovu. 16 Kwa maana palipo na wivu na ugomvi,* pana machafuko pia na kila jambo baya.^e

17 Lakini hekima inayotoka juu kwanza kabisa ni safi,^f kisha yenye kufanya amani,^g yenye usawaziko,^h tayari kutii, yenye kujaa rehema na matunda mema,ⁱ haina ubaguzi,^j na si ya kinafiki.^k 18 Zaidi ya hayo, tunda la uadilifu hupandwa katika hali zenye amani/ kwa* wale wanaofanya amani.^m

4 Ni nini chanzo cha vita na mapigano miongoni mweni? Je, havitokani na tamaa zenu za mwili zinazoendeleza pambano ndani yenu?^{*n} 2 Mnatamani, lakini hamna kitu. Mnaendelea kuua na kutamani kwa wivu, na bado hamwezi kupata. Mnaendelea kupigana na kufanya vita.^o Hamna kitu kwa sababu hamwombi. 3 Mnapoomba, hampokei kwa sababu mnaomba kwa kusudi baya, ili mvitumie kwa ajili ya tamaa zenu za mwili.

4 Enyi wazini,* je, hamjui kwamba urafiki na ulimwengu ni uadui na Mungu? Kwa hiyo, yeyote anayetaka kuwa rafiki ya ulimwengu anajifanya kuwa adui wa Mungu.^p 5 Au je, mnafikiri kwamba andiko linasema hivi bila sababu: "Roho ambayo imekaa ndani yetu huendelea kutamani kwa

3:14, 16 *Au labda, "tamaa ya kupata mambo makuu." 3:18 *Au labda, "na." 4:1 *Tnn., "ndani ya viungo vyenu." 4:4 *Au "Enyi msio waaminifu."

wivu"?^a **6** Hata hivyo, fadhili zisizostahiliwa ambazo Yeye hutoa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, linasema: "Mungu huwapinga wenye majivuno,^b lakini huwapa wanyenyekevu fadhili zisizostahiliwa."^c

7 Basi, jitiisheni kwa Mungu;^d lakini mpingeni Ibili-si,^e naye atawakimbia ninyi.^f

8 Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.^g Safishe ni mikonu yenu, ninyi wate-nda dhambi,^h na takaseni mioyo yenu,ⁱ ninyi mnaositasita.

9 Iweni na taabu na mwomboleze na kulia.^j Kicheko chenu na kigeuzwe kuwa maombolezo, na badala ya kuwa na shangwe mkate tamaa. **10** Jinyenyekezeni machoni pa Yehova,^{*k} naye atawainua.^l

11 Akina ndugu acheni kusemana kati yenu.^m Yeyote anayemsema vibaya ndugu au anayemhukumu ndugu yake husema vibaya juu ya sheria na kuihukumu sheria. Na ikiwa unaihukumu sheria, basi wewe si mtendaji wa sheria, bali ni mwamuzi. **12** Kuna mmoja tu ambaye ni Mpajisheria na Mwamuzi,ⁿ yule anayeweza kuokoa na kuangamiza.^o Lakini wewe ni nani ili umhukumu jirani yako?^p

13 Haya, basi, ninyi mnaosema: "Leo au kesho tutasafiri kwenda jiji fulani nasi tutakaa mwaka mmoja huko, tutafanya biashara na kupata faida,"^q **14** ingawa hamjui jinsi maisha yenu yatakavyokuwa kesho.^r Kwa maana ninyi ni ukungu unatokea kwa muda kidogo na kisha kutoweka.^s **15** Badala yake, mnapaswa kusema: "Yehova* akipe-

4:10, 15; 5:4 * Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 4

- a Mwa 6:5
Mwa 8:21
b Zb 138:6
c Met 3:34
1Pe 5:5
d Ebr 12:9
1Pe 2:17
1Pe 5:6
e Efe 4:27
Efe 6:11
f Mt 4:10, 11
Lu 4:13
g Isa 44:22
Isa 55:6, 7
h Isa 1:16
i 1Yo 3:3
j Yoe 2:12
k 2Nya 7:14
2Nya 33:12, 13
l Met 29:23
Mt 23:12
m Law 19:16
Met 17:9
n Isa 33:22
o Mt 10:28
p Mt 7:1
Lu 6:37
Ro 14:4
q Lu 12:18-20
r Zb 39:6
Met 27:1
Mhu 6:12
s Ayu 14:1, 2
Zb 102:3
1Pe 1:24

Safu ya 2

- a Mdo 18:21
Ebr 6:3
b Lu 12:47
Yoh 9:41
Yoh 15:22

SURA YA 5

- c Met 12:28
Lu 6:24
Lu 18:25
d Mt 6:19
Lu 12:33
e Eze 7:19
f Law 19:13
Kum 24:14, 15
Yer 22:13
Mal 3:5
g Yer 12:3
h Mt 24:3
i Kum 11:14
Yer 5:24
j Ebr 6:12
k 1Th 3:13
l 1Ko 4:5

nda,^a tutaishi na kufanya hili au lile." **16** Lakini sasa mnajivuna na kujigamba kwa kiburi. Majivuno yote ya namna hiyo ni maovu. **17** Kwa hiyo, ikiwa mtu anajua jinsi ya kufanya yaliyo sawa na bado hayafanyi, hiyo ni dhambi kwake.^b

5 Haya basi, enyi matajiri, lieni na kupiga mayowe kwa sababu ya taabu zitakazowapata.^c **2** Utajiri wenu umeoza, na mavazi yenu yameliwa na nondo.^{*d} **3** Dhahabu na fedha zenu zimeliwa na kutu, na kutu hiyo itakuwa ushahidi dhidi yenu nayo itakula miili yenu. Vitu mliyoweka akiba vitakuwa kama moto katika siku za mwisho.^e

4 Tazama! Mishahara ambayo hamjawalipa wafanyakazi waliovuna mashamba yenu, inaendelea kupaza kilio, na vilio vya kuomba msaada vya wavunaji vimefika masikioni mwa Yehova* wa majeshi.^f

5 Ninyi mmeishi kwa anasa na kwa ajili ya kutosheleza tamaa zenu duniani. Mmeinonesha mioyo yenu katika siku ya machinjo.^g **6** Mmemhukumu; mmemuua mwadilifu. Je, yeye hawapingi ninyi?

7 Basi, iweni na subira, aki-na ndugu, mpaka kuwapo kwa Bwana.^h Tazama! Mkulima huendelea kungojea matunda yenye thamani ya nchi, akiyashubiri mpaka mvua ya mape-ma na mvua ya baadaye inyeshi.ⁱ **8** Ninyi pia iweni na subira;^j imarisheni mioyo yenu, kwa sababu kuwapo kwa Bwana kumekaribia.^k

9 Msinung'unikiane,* akina ndugu, ili msihukumiwe.^l Ta-

5:2 * Aina ya wadudu. 5:9 * Au "Msizomeane; Msilalamikiane."

zama! Mwamuzi amesimama mbele ya milango. **10** Aki-na ndugu, fuateni mfano wa manabii waliopatwa na uovu^a na kuonyesha subira^b na ambao walisema katika jina la Yehova.*^c **11** Tazama! Tunawaona wale ambao wamevumilia kuwa wenye furaha.*^d Mmesikia kuhusu uvumilivu wa Ayubu^e na mmeona matokeo ambayo Yehova* alileta,^f kwamba Yehova* ni mwenye upendo mwororo sana^Δ na mwenye rehema.^g

12 Zaidi ya yote, akina ndugu, acheni kuapa kwa mbingu au kwa dunia au kwa kiapo kingine chochote. Bali acheni “Ndiyo” yenu iwe ndiyo, na “Siyo” yenu, siyo,^h ili msihukumiwe.

13 Je, kuna yeyote kati yenu aliye na matatizo? Na aendelee kusali.ⁱ Je, kuna yeyote mwenye roho changamfu? Na aimbe zaburi.^j **14** Je, kuna yeyote aliye mgonjwa kati yenu? Na awaite wazee^k wa kutaniko, nao wasali kwa

5:10, 11, 14, 15 *Angalia Nyongeza A5. 5:11 [#]Au “wamebarikiwa.” ^ΔAu “ni mwenye huruma sana.”

SURA YA 5

a Mt 5:12

b Ebr 6:12

c 2Nya 36:16

d Yak 1:2-4

e Ayu 1:20, 21

f Ayu 42:10

g Zb 103:8
Lu 6:36

h Mt 5:34-37

i Zb 50:15

j Kol 3:16

k Mdo 20:28, 35
1Pe 5:2

Safu ya 2

a Zb 141:5
Mk 6:13
Lu 10:34b 2Sa 12:13
Zb 32:5
Met 28:13
1Yo 1:9c 1Sa 12:18
1Fa 13:6

d 1Fa 17:1

e 1Fa 18:42, 45

f Gal 6:1

g 1Ti 4:16

ajili yake, wakimpaka mafuta^a katika jina la Yehova.* **15** Na sala ya imani itamponya huyo mgonjwa,[#] na Yehova* atamwinua. Pia, ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa.

16 Kwa hiyo ungameni waziwazi dhambi zenu^b kwa mtu na mwenzake na kusali kwa ajili ya mtu na mwenzake, ili mponywe. Dua ya mtu mwadilifu ina nguvu nyingi.*^c

17 Eliya alikuwa mtu mwenye hisia kama zetu, na bado aliposali kwa bidii mvua isinyeshe, haikunyeshwa juu ya nchi kwa miaka mitatu na miezi sita.^d **18** Naye akasali tena, na mbingu ikatoa mvua na nchi ikazaa matunda.^e

19 Ndugu zangu, yeyote kati yenu akipotoshwa kutoka katika kweli na mwingine amrudishe, **20** jueni kwamba yeyote anayemrudisha mtenda dhambi kutoka kwenye kosa^f la njia yake atamwokea* kutoka kwenye kifo naye atafunika dhambi nyingi.^g

5:15 [#]Au labda, “aliyechoka.” 5:16 *Tnn., “ina nguvu nyingi inapofanya kazi.” 5:20 *Au “ataokoa nafsi yake.”

BARUA YA KWANZA YA

PETRO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1, 2)
Kuzaliwa upya kwenye tumaini lililo hai (3-12)
Iweni watakatifu kama watoto watiifu (13-25)
- 2 Kuzeni hamu kwa ajili ya neno (1-3)

Mawe yaliyo hai yaliyojengwa kuwa nyumba ya kiroho (4-10)
Kuishi kama wageni katika ulimwengu (11, 12)
Ujitiisho unaofaa (13-25)
Kristo, kielelezo chetu (21)

- 3 Wake na waume (1-7)
Iweni na hisia-mwenzi; tafuteni amani (8-12)
Kuteseka kwa ajili ya uadilifu (13-22)
Muwe tayari kutetea tumaini lenu (15)
Ubatizo na dhamiri njema (21)
- 4 Kuishi kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, kama alivyofanya Kristo (1-6)
Mwisho wa mambo yote umekaribia (7-11)

- Kuteseka kwa kuwa Mkristo (12-19)
- 5 Lichungeni kundi la Mungu (1-4)
Muwe wanyenyekevu na mkeshe (5-11)
Mtupieni Mungu mahangaiko yenu yote (7)
Ibilisi ni kama simba anayenguruma (8)
Maneno ya kumalizia (12-14)

1 Petro, mtume^a wa Yesu Kristo, kwa wakaaji wa muda waliotawanyika katika Ponto, Galatia, Kapadokia,^b Asia, na Bithinia, kwa wale waliochaguliwa **2** kulingana na ujuzi wa awali wa Mungu aliye Baba,^c kwa kutakaswa kwa roho,^d kusudi wawe watiifu na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo:^e

Na mwongezewe fadhili zizozostahiliwa na amani.

3 Asifiwe Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwa maana kulingana na rehema yake kubwa alituzaa sisi upya^f kwenye tumaini lililo hai^g kupitia ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu,^h **4** kwenye urithi usioharibika na usio na unajisi na usioifia. Urithi huo umewekwa aki-ba mbinguni kwa ajili yenu,ⁱ **5** ninyi mnaolindwa kwa nguvu za Mungu kupitia imani kwa ajili ya wokovu ulio tayari kufunuliwa katika kipindi cha mwisho cha wakati. **6** Kwa sababu ya jambo hilo mnashangilia sana, ingawa kwa muda mfupi, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu mbalimbali,^k **7** ili sifa iliyotaribiwa ya imani yenu,^l iliyo na thamani kubwa zaidi

SURA YA 1

a Mt 10:2

b Mdo 2:5, 9

c Ro 8:29

d 2Th 2:13

e Ebr 12:22, 24

f 1Pe 1:23

g Ufu 20:6

h 1Ko 15:20

i 1Ko 15:53
2Ti 1:10
1Pe 5:4j Yoh 14:2
2Ti 4:8k 2Ko 4:17
2Ti 3:12

l Yak 1:2, 3

Safu ya 2

a 2Th 1:7

b Ro 6:22

c Mt 13:17

d Da 9:24-27

e Isa 53:5

kuliko dhahabu ambayo huharibika ijapokuwa inajaribiwa* kwa moto, ipatikane kuwa sababu ya sifa na utukufu na heshima wakati wa ufufuo wa Yesu Kristo.^a **8** Mnampenda ingawa hamkumwona kamwe. Ijapokuwa hammwoni sasa, bado mnaonyesha imani katika yeye na mnashangilia sana kwa shangwe isiyozeleka na iliyotukuka, **9** huku mkifikia lengo la* imani yenu, wokovu wenu.^{#b}

10 Kuhusu wokovu huu, manabii waliotoa unabii kuhusu fadhili zizozostahiliwa zilizokusudiwa kwa ajili yenu, walifanya uchunguzi kwa bidii na kutafuta kwa uangalifu.^c **11** Waliendelea kuchunguza wakati hususa au majira ambayo roho iliyokuwa ndani yao ilikuwa ikionyesha kuhusu Kristo^d ilipokuwa ikitoa ushahidi mapema kuhusu mateso ya Kristo^e na kuhusu utukufu ambao ungefuata. **12** Walifunuliwa kwa mba hawakuwa wakijihudumia wenyewe, bali walikuwa wakiwahudumia ninyi, kwa mambo ambayo sasa mmeta-

1:7 *Au "inasafishwa." 1:9 *Au "mradi wa." #Au "wokovu wa nafsi zenu."

ngaziwa na wale ambao wali-watangazia habari njema kwa roho takatifu iliyotumwa kutoka mbinguni.^a Malaika wanatamani kuchungulia ndani ya mambo hayo.

13 Kwa hiyo kazeni akili zenu kwa ajili ya utendaji,^b tunzeni akili zenu kwa ukamili;^c kazeni tumaini lenu juu ya fadhili zisizostahiliwa zitakazoletwa kwenu wakati wa ufunuo wa Yesu Kristo. **14** Kama watoto watiifu, acheni kufinyangwa* na tamaa mlizokuwa nazo zamani katika hali yenu ya kutojua, **15** lakini iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote kama Yule Mtakatifu aliyewaita ninyi,^d **16** kwa maana imeandikwa: "Lazima muwe watakatifu, kwa sababu mimi ni mtakatifu."^e

17 Na ikiwa mnamwitia Baba ambaye huhukumu bila ubaguzi^f kulingana na matendo ya kila mmoja, jien-desheni kwa kuogopa^g wakati ambao ninyi ni wakaaji wa muda. **18** Kwa maana mnajua kwamba mliwekwa huru*^h kutoka kwenye mwenendo wenu usio na faida ambao mlipokea kutoka kwa mababu zenu,ⁱ si kwa vitu vyenye kuharibika, kwa fedha au dhahabu, **19** bali ilikuwa kwa damu yenye thamani,^j kama ile ya mwanakondoo asiye na dosari^j na asiye na doa, ile ya Kristo.^k **20** Ni kweli, yeye alijulikana mape-ma kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu,^l lakini alifunuliwa mwishoni mwa nyakati kwa ajili yenu.^m **21** Kupitia

1:14 *Au "kufanyizwa kulingana." 1:18 *Tnn., "mililipiwa fidia; mlikombolewa." *Au "kutokana na desturi."

SURA YA 1

a Yoh 15:26

Mdo 2:4

b Lu 12:35

c Efe 5:17

1Pe 4:7

d Kum 28:9

Ro 12:1

Ebr 12:14

e Law 11:44

Law 19:2

Law 20:7, 26

f Kum 10:17

g 2Ko 7:1

h 1Ko 6:20

i Isa 53:12

Ebr 9:14

j Kut 12:5

Law 22:20

Yoh 1:29

k 1Ko 5:7

l Yoh 17:5

Efe 1:4

m Kol 1:26, 27

Safu ya 2

a Yoh 14:6

b Mdo 2:24

c Ebr 2:9

d Ro 12:9

1Yo 3:17

e 1Ti 1:5

f Yoh 3:3

2Ko 5:17

1Pe 1:3

1Yo 3:9

g Yoh 3:6

h Yoh 6:63

Yak 1:18

i Isa 40:6-8

j Tit 1:3

SURA YA 2

k Gal 5:16

Yak 1:21

l Mk 10:15

m 2Ti 3:15

n Isa 53:3

Yoh 19:15

o Zb 118:22

Isa 42:1

Mt 21:42

Mdo 4:11

p Efe 2:21

yeye mnamwamini Mungu,^a yule aliyemfufua kutoka kwa wafu^b na kumpa utukufu,^c ili imani na tumaini lenu liwe katika Mungu.

22 Sasa kwa sababu mmejitakasa wenyewe* kwa kuwa watiifu kwa ile kweli na hivyo kuwa na upendo wa kindugu^d bila unafiki, pendenani sana kutoka moyoni.^e **23** Kwa maana mmezaliwa upya,^f si kupitia mbegu* yenye kuharibika, bali kupitia ile isiyoharibika,^g kupitia neno la Mungu aliye hai na anayedumu.^h **24** Kwa maana "wote wenye mwili ni kama nyasi, na utukufu wao wote ni kama ua la shambani; nyasi hukauka, na ua huanguka, **25** bali neno la Yehova* linadumu milele."ⁱ Na "neni" hilo ni habari njema mliyotangaziwa.^j

2 Basi, acheni ubaya wote^k na udanganyifu na unafiki na wivu na masengenyo. **2** Kama watoto wachanga waliozaliwa hivi karibuni,^l kuzeni hamu kwa ajili ya maziwa yasiyochanganywa na kitu* ya lile neno, ili kupitia hayo mkue kufikia wokovu,^m **3** mradi tu mmeonja na kuona kwamba Bwana ni mwenye fadhili.

4 Mkimjia yeye, jiwe lililo hai lililokataliwa na wanadamuⁿ bali lililochaguliwa na lenye thamani kwa Mungu,^o **5** ninyi wenyewe pia kama mawe yaliyo hai mnajengwa kuwa nyumba ya kiroho^p kusudi muwe ukuhani mtakatifu, ili kutoa dhabihu za

1:22 *Au "mmezitakasa nafsi zenu." 1:23 *Yaani, mbegu inayoweza kuzaa, au inayotokeza matunda. 1:25 *Angalia Nyongeza A5. 2:2 *Au "maziwa safi; maziwa halisi."

kiroho^a zenye kukubalika kwa Mungu kupitia Yesu Kristo.^b **6** Kwa maana Andiko linasema: "Tazama! Ninaweka katika Sayuni jiwe lililochaguliwa, jiwe la pembeni la msingi lenye thamani, na yeyote anayeonyesha imani katika hilo hatakata tamaa kamwe."^c

7 Kwa hiyo, yeye ni mwenye thamani kwenu, kwa sababu ninyi ni waamini; lakini kwa wale wasioamini, "jiwe ambalo wajenzi walilikataa^d limekuwa jiwe kuu la pembeni"^e

8 na "jiwe la kukwaza na mwamba wa kuangusha."^f Wanajikwaa kwa sababu hawatii lile neno. Waliwekwa rasmii pia kwa kusudi hilo. **9** Lakini ninyi ni "jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu,^g na watu walio mali ya pekee,^h ili mtangaze kotekote sifa bora"ⁱ za Yule aliyewaita kutoka katika giza kuingia katika nuru yake ya ajabu.^j **10** Kwa kuwa wakati fulani ninyi hamkuwa watu, lakini sasa ninyi ni watu wa Mungu;^k hamkuwa mmeonyeshwa rehema, lakini sasa mmeonyeshwa rehema.^l

11 Wapendwa, ninawahimiza ninyi kama wageni na waakaaji wa muda^m kwamba mwendeele kujiepusha na tamaa za mwili,ⁿ ambazo hupigana vita nanyi.^o **12** Dumisheni mwendo wenu ukiwa mzuri kati ya mataifa,^p ili wanapowashutumua kuwa watenda dhambi, washuhudie kwa macho yao matendo yenu mazuri^q na hivyo wantukuze Mungu katika siku ya ukaguzi wake.

2:6 *Tnn., "hataabika." 2:7 *Tnn., "kichwa cha pembeni." 2:9 *Yaani, sifa zake nzuri na matendo mazuri. 2:11 *Au "na nafsi zenu."

SURA YA 2

a Ebr 13:15

b Ro 12:1

c Isa 28:16

d Zb 69:8

e Zb 118:22

Mt 21:42

Lu 20:17

Mdo 4:11

f Isa 8:14

g Ufu 5:10

Ufu 20:6

h Kut 19:5, 6

Kum 7:6

Kum 10:15

Mal 3:17

i Isa 43:20, 21

j Efe 5:8

Kol 1:13

k Ho 1:10

Mdo 15:14

Ro 9:25

l Ho 2:23

m 1Pe 1:17

n Ro 8:5

Gal 5:24

o Gal 5:17

Yak 4:1

p Ro 12:17

1Ti 3:7

q Mt 5:16

Yak 3:13

Safu ya 2

a Ro 13:1

Efe 6:5

Tit 3:1

b 1Pe 2:17

c Ro 13:3, 4

d Tit 2:7, 8

e Gal 5:1

f Gal 5:13

g 1Ko 7:22

h Law 19:32

Ro 12:10

Ro 13:7

i 1Yo 2:10

1Yo 4:21

j Zb 111:10

Met 8:13

Zko 7:1

k Met 24:21

l Efe 6:5

Kol 3:22

1Ti 6:1

Tit 2:9

m Ro 13:5

n 1Pe 4:15

o Mt 5:10

Mdo 5:41

1Pe 4:14

p 1Pe 3:18

q Mt 16:24

Yoh 13:15

r Yoh 8:46

Ebr 4:15

13 Kwa ajili ya Bwana jitii-sheni wenyewe kwa kila kitu kilichofanywa na binadamu,^a iwe ni kwa mfalme^b akiwa mkubwa **14** au kwa magavana wakiwa kama wame-tumwa naye kuwaadhibu watenda maovu lakini kuwasifu wanaotenda mema.^c **15** Kwa maana ni mapenzi ya Mungu kwamba kwa kutenda mema mnyamazishe* maneno ya kijinga ya watu wasio na akili.^d **16** Iweni kama watu huru,^e mkitumia uhuru wenu, si kama kifuniko* cha kufanya mabaya,^f bali kama watumwa wa Mungu.^g **17** Wa-heshimuni watu wa namna zote,^h upendeni ushirika mzima wa akina ndugu,ⁱ mwogopeni Mungu,^j mheshimuni mfalme.^k

18 Watumishi na wajitiishi kwa mabwana wao kwa woga unaofaa,^l si kwa wale tu walio wema na wapole, bali pia kwa wale ambao ni wagumu kupendeza. **19** Kwa maana inakubalika ikiwa mtu anavumilia taabu* na kuteseka isivyo haki kwa sababu ya dhamiri kwa Mungu.^m **20** Kwa maana kuna faida gani ikiwa mnavumilia mnapopigwa kwa kufanya dhambi?ⁿ Lakini ikiwa mnavumilia mateso kwa sababu ya kufanya mema, jambo hilo linakubalika kwa Mungu.^o

21 Kwa kweli, mliitwa kwenye mwendo huu, kwa sababu hata Kristo aliteseka kwa ajili yenu,^p akiwaachia ninyi kielelezo ili mfuate hatua zake kwa ukaribu.^q **22** Yeye hakufanya dhambi,^r wala udanganyifu haukupatikana kinywani

2:13 *Au "shirika la kibinadamu." 2:15 *Tnn., "mzibe." 2:16 *Au "kisingizio." 2:17 *Tnn., "undugu." 2:19 *Au "huzuni; maumivu."

mwake.^a **23** Alipokuwa akikutukanwa,^{*b} hakujibu kwa kutukana.^{#c} Alipokuwa akiteseka,^d hakutoa vitisho, bali alijikabidhi mkononi mwa Yule anayehukumu^e kwa uadilifu.

24 Yeye mwenyewe alichukua dhambi zetu^f katika mwili wake mwenyewe juu ya mti,^g ili tufe kuhusiana* na dhambi na tuishi kuhusiana* na uadilifu. Na “kwa vidonda vyake mliponywa.”^h **25** Kwa maana mlikuwa kama kondoo wanaopotea njia,ⁱ lakini sasa mmerudi kwa mchungaji^j na mwanagalizi wa nafsi zenu.*

3 Vivyo hivyo, ninyi wake, jitiisheni kwa waume zenu,^k ili ikiwa kuna wale wasiotii lile neno, wavutwe bila neno kupitia mwenendo wa wake zao,^l **2** kwa sababu wameshuhudia kwa macho yao mwenendo wenu ulio safi kiadili^m pamoja na heshima kubwa. **3** Kujipamba kwenu kusiwe kwa nje—kusuka nywele na kuvaa mapambo ya dhahabuⁿ au mavazi bora— **4** bali kuwe yule mtu wa siri wa moyoni katika mapambo yasiyoharibika ya roho ya utulivu na ya upole,^o ambayo ni ya thamani kubwa machoni pa Mungu. **5** Kwa maana hapo zamani ndivyo walivyokuwa wakijipamba wale wanawake watakatifu, waliomtumaini Mungu, wakijitiisha kwa waume zao, **6** kama Sara alivyomtii Abrahamu, akimwita bwana.^p Nanyi mmekuwa watoto wake, mradi tu mnaendelea kutenda mema, bila kuogopa.^q

7 Enyi waume, vivyo hivyo endeleeni kukaa nao kulinga-

2:23 *Au “akishutumiwa.” #Au “hakushutumu.” 2:24 *Au “tuachane.” 2:25 *Au “wa uhai wenu.”

SURA YA 2

a Isa 53:9
b Mt 27:39
c Isa 53:7
Ro 12:21
d Ebr 5:8
e Yer 11:20
Yoh 8:50
f Law 16:21
g Flp 2:8
h Isa 53:5
i Isa 53:6
j Zb 23:1
Isa 40:11

SURA YA 3

k Ro 7:2
1Ko 11:3
Efe 5:22
l 1Ko 7:16
m 1Pe 2:12
n Met 11:22
o Efe 4:24
Kol 3:10, 12
1Ti 2:9, 10
p Mwa 18:12
Efe 5:33
q Met 3:25
Flp 1:28

Safu ya 2

a Efe 5:25
b Gal 3:28
c 1Ko 1:10
Flp 2:2
d Ro 12:10
e Ro 15:5
Kol 3:12
f Ro 12:17
1Th 5:15
g 1Pe 2:23
h Ro 12:14
1Ko 4:12
i Yak 3:8
j Met 8:13
k 3Yo 11
l 1Th 5:13
Yak 3:17
m 1Yo 3:22
n Zb 34:12-16
o Ro 13:3, 4
p Mt 5:11, 12
Mdo 5:41
1Pe 2:19
q Mt 10:28
r Met 15:1
2Ti 2:24, 25
Tit 3:1, 2
s Kol 4:6

na na ujuzi.* Wapeni heshima^a kama chombo dhaifu zaidi, yaani, mwanamke, kwa kuwa wao pia ni warithi pamoja nanyi^b wa pendeleo lililostahiliwa la uzima, ili sala zenu zisizuwe.

8 Mwishowe, ninyi nyote fikirini kwa upatano,^{*c} muwe na hisia-mwenzi, upendo wa kindugu, huruma nyororo,^d na unyenyekevu.^e **9** Msilipe ubaya kwa ubaya^f au matukano kwa matukano.^g Badala yake, lipeni kwa baraka,^h kwa sababu mliitwa kwenye mwendo huu, ili mrithi baraka.

10 Kwa maana “yeyote anayependa uzima na kuona siku zilizo njema, lazima aulinde ulimi wake usiseme mabayaⁱ na midomo yake isiseme udanganyifu. **11** Na aache mabaya,^j atende mema;^k na atafute amani na kuifuatilia.^l **12** Kwa maana macho ya Yehova* yanawatazama waadilifu, na masikio yake yanasikiliza dua yao,^m lakini uso wa Yehova* uko dhidi ya wale wa-naotenda maovu.”ⁿ

13 Kwa kweli, ni nani atakayewadhuru mkifanya yaliyo mema kwa bidii?^o **14** Lakini hata mkiteseka kwa ajili ya uadilifu, ninyi ni wenye furaha.^p Hata hivyo, msiogope kile wanachokiogopa,* wala msiwe na wasiwasi.^q **15** Bali mtakaseni Kristo kuwa Bwana katika mioyo yenu, sikuzote mkiwa tayari kujitetea mbele ya kila mtu anayewauliza sababu ya tumaini mlilo nalo, lakini mkifanya hivyo kwa upole^r na heshima kubwa.^s

3:7 *Au “mkiwafikiria na kuwajali; kuwaelewa.” 3:8 *Au “kwa umoja wa akili.” 3:12 *Angalia Nyongeza A5. 3:14 *Au labda, “msiogope vitisho vyao.”

16 Iweni na dhamiri nje-ma,^a ili katika kila jambo ambalo wanasema vibaya dhidi yenu, wale wanaosema vibaya dhidi yenu waaibishwe^b kwa sababu ya mweneo wenu mzuri mkiwa wafuasi wa Kristo.^c 17 Kwa maana ni afadhali kuteseka kwa sababu mnatenda mema,^d ikiwa ni mapenzi ya Mungu kuruhusu jambo hilo, kuliko kuteseka kwa sababu mnatenda maovu.^e 18 Kwa maana Kristo alikufa mara moja kwa wakati wote kwa ajili ya dhambi,^f mtu waadilifu kwa ajili ya wasio waadilifu,^g ili awaongoze ninyi kwa Mungu.^h Aliuawa katika mwili,ⁱ lakini akafanywa kuwa hai katika roho.^j 19 Na katika hali hiyo alienda na kuwahabirira roho walio gerezani,^k 20 ambao mwanzoni hawakuwa watiifu Mungu alipokuwa akingoja kwa subira* katika siku za Noa,^l safina ilipokuwa ikijengwa,^m ambayo ndani yake watu wachache, yaani, nafsi nane,ⁿ walichukuliwa salama kupitia maji.ⁿ

21 Ubatizo, ambao unalingana na hili, unawaokoa ninyi sasa pia (si kwa kuondoa uchafu wa mwili, bali kwa ombi linalotolewa kwa Mungu ili kupata dhamiri njema),^o kupitia ufufuo wa Yesu Kristo. 22 Yeye yuko kwenye mkono wa kuume wa Mungu,^p kwa maana alienda mbinguni, nao malaika na mamlaka na nguvu vilitiishwa kwake.^q

4 Kwa kuwa Kristo aliteseka katika mwili,^r ninyi pia jii-marisheni kwa mwelekeo uleule wa akili,* kwa sababu

3:20 *Tnn., "subira ya Mungu ilikuwa ikingoja." #Au "watu wanane." 4:1 *Au "azimio lilelile; uamuzi uleule."

SURA YA 3

a Mdo 23:1
Mdo 24:16
1Ti 1:5
1Ti 1:18, 19
1Ti 3:9
b Tit 2:8
c Ro 12:21
1Pe 2:12
d 2Ko 1:7
Kol 1:24
e 1Pe 4:15
f Ebr 9:28
g Ro 5:6
h 2Ko 5:18
i 1Ko 15:50
j 1Ti 3:16
k 2Pe 2:4
Yud 6
l Mwa 6:2, 3
m Mwa 6:14
n Mwa 7:13, 23
o Ebr 9:14
Ebr 10:22
p Zb 110:1
Mdo 7:55
Ebr 10:12
q Mt 28:18
1Ko 15:25
Efe 1:20, 21
Flp 2:9, 10
Ebr 1:6

SURA YA 4

r Flp 2:8

Safu ya 2

a Ro 6:11
Kol 3:5
1Yo 3:6
b 2Ko 5:15
c Gal 2:20
Efe 5:17
d Tit 3:3
e Ro 13:13
1Ko 5:11
Gal 5:19, 21
Efe 4:17-19
f 1Pe 3:16
g Mdo 10:42
Mdo 17:31
ZTi 4:1
Ufu 20:12
h Efe 2:1
i Ro 12:3
1Ti 3:2
Tit 2:6
j Kol 4:2
k Kol 3:14
l Met 10:12
Met 17:9
1Ko 13:4, 7
m 2Ko 9:7
Ebr 13:2
n Ro 12:6-8

mtu ambaye ameteseka katika mwili ameachana na dhambi,^a 2 ili aishi wakati wake uliobaki katika mwili, si kwa ajili ya tamaa za wanadamu tena,^b bali kwa ajili ya mapenzi ya Mungu.^c 3 Kwa maana wakati uliopita uliwatosha kufanya mapenzi ya mataifa,^d mlipofanya vitendo vya mwenendo mpotovu,^e uchu, kunywa kupita kiasi, karamu zenye vurugu,^f mashindano ya kunywa, na ibada za sanamu zenye kuchukiza.^e 4 Wanashangaa kwa sababu hamwendelei kukimbia pamoja nao katika mwendo uliooza wa upotovu, basi wanawatukana ninyi.^f 5 Lakini watu hao watatoa hesabu kwa yule aliye tayari kuhukumu walio hai na waliokufa.^g 6 Kwa kweli, hiyo ndiyo sababu habari njema ilitangazwa kwa wafu pia,^h ili ingawa wanahukumiwa katika mwili kwa maoni ya wanadamu, waishi kwa kupatana na roho kwa maoni ya Mungu.

7 Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia. Kwa hiyo, iweni na utimamu wa akili,ⁱ na kukesha* kuhusiana na sala.^j 8 Zaidi ya mambo yote, pendenani sana,^k kwa sababu upendo hufunika dhambi nyingi.^l 9 Mkaribishane bila kunung'unika.^m 10 Kwa kadiri ambayo kila mmoja amepokea zawadi, itumieni kuhudumiana kama wasimamizi wazuri wa fadhili zizizostahiliwa za Mungu zinazoonyeshwa kwa njia mbalimbali.ⁿ 11 Yeyote akisema, na afanye hivyo

4:3 *Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki, *a-sel'gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. #Au "karamu za kupindukia." 4:7 *Au "muwe chonjo; muwe macho."

kana kwamba^c anasema maneno matakatifu kutoka kwa Mungu; yeyote akihudumu, na afanye hivyo kama anayetegemea nguvu ambazo Mungu hutoa;^a ili katika mambo yote Mungu atukuzwe^b kupitia Yesu Kristo. Utukufu na nguvu ni zake milele na milele. Amina.

12 Wapendwa, msishangazwe na majaribu makali* yanayowapata,^c kana kwamba mnapatwa na jambo geni. **13** Badala yake, endeleeni kushangilia^d kwa kadiri ambayo ninyi ni washiriki katika mateso ya Kristo,^e ili mshangilie na kuwa na shangwe sana pia wakati wa ufunuo wa utukufu wake.^f **14** Ikiwa mnashutumiwa* kwa ajili ya jina la Kristo, ninyi ni wenye furaha,^g kwa sababu roho ya utukufu, yaani roho ya Mungu, inatulia juu yenu.

15 Hata hivyo, yeyote kati yenu asiteseke kwa sababu yeye ni muuaji au mwizi au mkosaji au mtu anayejiingiza katika mambo ya watu wengine.^h **16** Lakini yeyote akite-seka kwa sababu ni Mkristo, asione aibu,ⁱ bali na aendeele kumtukuzwa Mungu huku akilibeba jina hili. **17** Kwa maana ni wakati uliowekwa wa hukumu kuanza na nyumba ya Mungu.^j Sasa ikiwa inaanza na sisi kwanza,^k basi matokeo kwa wale wasiotii habari njema ya Mungu yatakuwaje?^l **18** "Na ikiwa mtu mwadilifu anaokolewa kwa shida, itakuwaje kwa mtu asiyemwogopa Mungu na mtenda dhambi?"^m **19** Hivyo basi, acheni wale wanaoteseka kwa ku-

4:12 *Au "majaribu kama moto." 4:14 *Au "mnatukanwa."

SURA YA 4

a Isa 12:2
Efe 3:20

b 1Ko 10:31

c 1Pe 5:9

d Mdo 5:41

Yak 1:2

e Ro 8:17

2Ko 4:10

2Ti 3:12

f 1Pe 1:7

g Yak 1:12

Yak 5:11

h 1Ti 5:13

1Pe 2:20

i Kol 1:24

Ebr 12:2

j Ebr 3:6

k 1Ko 11:32

l 2Th 1:7, 8

m Met 11:31

Mt 7:13, 14

Safu ya 2

a 2Ti 1:12

SURA YA 5

b Ro 8:18

c Isa 40:11

Yoh 21:16

Mdo 20:28

d Yoh 10:11

e 1Ti 3:2, 3

f 2Ko 1:24

g Flp 3:17

h Ebr 13:20

i 1Ko 9:25

2Ti 4:8

1Pe 1:3, 4

j Efe 5:21

Yak 3:17

k Met 3:34

Isa 57:15

Yak 4:6

l Mt 23:12

Lu 14:11

m Mt 6:25

n Zb 55:22

o 1Th 5:6

p Lu 22:31

fanya mapenzi ya Mungu waeendeele kujikabidhi wenyewe* kwa Muumba mwaminifu wanaopotenda mema.^a

5 Kwa hiyo, nikiwa mzee pia, shahidi wa mateso ya Kristo, na mshiriki wa utukufu utakaofunuliwa,^b ninawasihi* wazee miongoni mweni: **2** Lichungeni kundi la Mungu^c lililo chini ya utunzaji wenu, mkiwa waangalizi,* si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari mbele za Mungu;^d si kwa kupenda pato lisilo la haki,^e bali kwa hamu; **3** si kupiga ubwana juu ya wale ambao ni urithi wa Mungu,^f bali kuwa vielelezo kwa kundi.^g **4** Na mchungaji mkuu^h atakapofunuliwa, mtapokea taji la utukufu lisilofifia.ⁱ

5 Vivyo hivyo, enyi vijana, jitiisheni kwa wanaume wazee.*^j Lakini ninyi nyote mteendeele kwa* unyenyekevu,^Δ kwa sababu Mungu huwapinga wenye majivuno, lakini huwapa wanyenyekevu fadhili zisizostahiliwa.^k

6 Kwa hiyo, jinyenyekezeni chini ya mkono wenye nguvu wa Mungu, ili awainue kwa wakati unaofaa,^l **7** huku mkitupa mahangaiko* yenu yote juu yake,^m kwa sababu yeye anawajali ninyi.ⁿ **8** Tunzeni akili zenu, iweni waangalifu!^o Adui yenu, Ibilisi, anatembea huku na huku kama simba anayenguruma, akitafuta kummeza mtu.*^p

4:19 *Au "kuzikabidhi nafsi zao." 5:1 *Au "ninawahimiza." 5:2 *Au "mkililinda kwa makini." 5:5 *Au "wazee." *Au "mjifunge; mjivike." ΔAu "unyenyekevu wa akili." 5:7 *Au "matatizo; wasiwasi wenu wote." 5:8 *Au "akitafuta mtu ili ammeze."

9 Lakini chukueni msimamo dhidi yake,^a mkiwa imara katika imani, mkijua kwamba mateso yaleyale yanaupata ushirika mzima wa ndugu zenu* ulimwenguni.^b **10** Lakini, baada ya kuteseka kwa muda mfupi, Mungu wa fadhili zote zisizostahiliwa, aliyewaita kwenye utukufu wake wa milele^c katika muungano na Kristo, yeye mwenyewe atamaliza mazoezi yenu. Atawafanya muwe imara,^d atawatia nguvu,^e atawapa msingi imara. **11** Na awe na nguvu milele. Amina.

5:9 *Tnn., “undugu wenu.”

SURA YA 5

a Efe 6:11
Yak 4:7

b Mdo 14:22
2Ti 3:12

c 2Ko 4:17
1Th 2:12

d 2Th 2:16,17

e Efe 6:10

Safu ya 2

a Mdo 15:27

b Mdo 12:12

12 Kupitia Silvano,^{*a} ambaye ninamwona kuwa ndugu mwaminifu, nimewaandikia kwa maneno machache, ili kuwatie moyo na kutoa ushahidi kwa bidii kwamba hizi ndizo fadhili zisizostahiliwa za Mungu. Simameni imara katika fadhili hizo. **13** Mwanamke aliye Babiloni, aliyechaguliwa kama ninyi, anawatumia salamu zake, na vilevile Marko,^b mwanangu. **14** Salimianeni kwa busu la upendo.

Na muwe na amani ninyi nyote mlio katika muungano na Kristo.

5:12 *Pia anaitwa Sila.

BARUA YA PILI YA

PETRO

YALIYOMO

- 1 Salamu (1)
Fanyeni mwito wenu uwe hakika (2-15)
Sifa zinazoongezwa kwenye imani (5-9)
Neno la kinabii lafanywa hakika zaidi (16-21)
- 2 Walimu wa uwongo watatokea (1-3)
Hukumu dhidi ya walimu wa uwongo ni hakika (4-10a)
Malaika watupwa ndani ya Tartaro (4)

- Gharika; Sodoma na Gomora (5-7)
Tabia za walimu wa uwongo (10b-22)
- 3 Wadhuhaki wapuuza uharibifu unaokuja (1-7)
Yehova hakawii (8-10)
Fikirieni mnapaswa kuwa watu wa aina gani (11-16)
Mbingu mpya na dunia mpya (13)
Jilindeni ili msipotoshwe (17, 18)

1 Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale ambao wamepata imani, yenye thamani kama yetu* kupitia uadilifu wa Mu-

1:1 *Au “imani waliyo nayo katika pendeleo lililo sawa na letu.”

Safu ya 2

SURA YA 1

a Kol 1:9

ngu wetu na Mwokozi wetu Yesu Kristo:

2 Na mwongezewe fadhili zisizostahiliwa na amani kwa ujuzi sahihi^a kumhusu Mungu na kumhusu Yesu Bwana wetu, **3** kwa maana nguvu

zake za kimungu zimetupatia* mambo yote yanayoleta uzi- ma na ujitoaji-kimungu# kupitia ujuzi sahihi kumhusu Yule ambaye alituita^a kwa utukufu wake na wema wa adili. **4** Kupitia mambo haya ametupatia* ahadi zenye thamani na zilizo bora,^b ili kupitia hizo muwe washiriki katika asili ya kimungu,^c mkiwa mmeponyoka kutoka katika uharibifu wa ulimwengu unaosababishwa na tamaa mbaya.#

5 Kwa sababu hii, jitahidini kabisa^d kuongeza kwenye imani yenu wema wa adili,^e kwenye wema wenu wa adili ujuzi,^f **6** kwenye ujuzi wenu kujizuia,* kwenye kujizuia*^g kwenye uvumilivu, kwenye uvumilivu wenu ujitoaji-kimungu,^h **7** kwenye ujitoaji-kimungu# wenu upendo wa kindugu, kwenye upendo wenu wa kindugu upendo.ⁱ **8** Kwa maana mambo hayo yakiwa ndani yenu na kufurika, yatawazuia msiwe wasiotenda ama wasiozaza matunda*^j kuhusiana na ujuzi sahihi kumhusu Bwana wetu Yesu Kristo.

9 Kwa maana yeyote asiye na mambo hayo ni kipofu, na amefunga macho yake yasione nuru,^k naye amesahau kutakaswa kwake kutoka kwenye dhambi zake^l za zamani za kale. **10** Kwa hiyo, akina ndugu, jitahidini hata zaidi ili kufanya mwito^m na kuchaguliwa kwenu kuwe ha-

1:3 *Au "zimetupatia bila malipo." 1:3, 6, 7 #Angalia Kamusi, uku. 2012. 1:4 *Au "ametupatia bila malipo." #Au "uchu." 1:6 *Au "kujidhibiti; kujiweza." 1:8 *Au "wasiopata matokeo mazuri." 1:9 *Au labda, "kipofu, asiyeona mbali."

SURA YA 1

a Yoh 17:3

b Lu 22:29, 30
Yoh 14:2
Gal 3:29c 1Ko 15:53
1Pe 1:3, 4
1Yo 3:2
Ufu 20:6d Flp 2:12
2Ti 2:15
Ebr 4:11
Yud 3

e Flp 4:8

f Yoh 17:3
Ebr 5:14g 1Ko 9:25
2Ti 2:24

h 2Pe 2:9

i 1Th 4:9

j Tit 3:14

k 1Yo 2:9
Ufu 3:17

l Ebr 9:14

m Ebr 3:1

Safu ya 2

a 2Ti 4:7, 8

b Da 2:44

c Lu 16:9
Yoh 3:5

d 2Ko 5:1

e Ro 15:15
Yud 5

f Yoh 21:18

g Mt 17:2
Mk 9:2
Lu 9:29h Zb 2:7
Mt 17:1, 5
Mk 9:7
Lu 9:35

kika kwa ajili yenu wenyewe, kwa maana mkiendelea kufanya mambo hayo, hamtashindwa kamwe.^a **11** Kwa kweli, hivyo ndivyo mtakavyowezeshwa* kwa wingi kuingia katika Ufalme wa milele^b wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.^c

12 Kwa sababu hiyo sikuzote ninakusudia kuwakuambusha mambo haya, ingawa mnyajua na mko imara katika kweli iliyi ndani yenu.

13 Lakini ninaona inafaa, maadamu niko katika maskani hii,^d kuwachochea kwa kuwakuambusha,^e **14** kama ninavyojuua kwamba maskani yangu itaondolewa hivi karibuni, kama vile pia Bwana wetu Yesu Kristo alivyonyesha.^f **15** Sikuzote nitafanya yote ninayoweza ili nitakapoondoka, ninyi wenyewe muweze ku yakumbuka* mambo hayo.

16 Hapana, hatukuwajulisha kuhusu nguvu na kuwapo kwa Bwana wetu Yesu Kristo kwa kufuata hadithi za uwongo zilizotungwa kwa werrevu, badala yake, tulijio- nea kwa macho fahari yake.^g

17 Kwa maana alipokea kutoka kwa Mungu Baba heshima na utukufu alipoambiwa maneno kama haya* kwa utukufu wenye fahari: "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ambaye mimi mwenyewe nimemkubali."^h **18** Ndiyo, maneno hayo tuliyasikia yakitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika ule mlima mta- katifu.

1:11 *Au "mtakavyoongezewa." 1:13 *Au "hema hili," yaani, mwili wake wa duniani. 1:15 *Au "kuyataja." 1:17 *Tnn., "sauti kama hii."

19 Basi tuna neno la kinabii likiwa limefanywa hakika zaidi, nanyi mnafanya vema kuli-kazia uangalifu kama vile taa^a inayoangaza mahali penye giza (mpaka siku ipambazuke na nyota ya mchana^b ichomoz) moyoni mwenu. **20** Kwa kuwa kwanza mnajua kwamba hakuna unabii wa Andiko unaotokana na fasiri yoyote ya kibinafsi. **21** Kwa maana unabii haukuletwa wakati wowote kwa mapenzi ya mwanaadamu,^c bali wanadamu walisema yaliyotoka kwa Mungu kama walivyoongozwa* na roho takatifu.^d

2 Hata hivyo, kulikuwa pia na manabii wa uwongo miongoni mwa watu, kama vile pia kutakavyokuwa na walimu wa uwongo miongoni mwenu.^e Hawa wataingiza kimyakimya madhehebu yenye kuharibu, na hata watamkana bwana aliyewanua,^f na kujiletea maangamizi ya haraka. **2** Zaidi ya hayo, wengi watafuata mwenendo wao mpotovu,^g na kwa sababu yao ile njia ya kweli itatukanwa.^h **3** Pia, watawatumia ninyi vibaya kwa pupa wakisema maneno ya uwongo. Lakini hukumu yao iliyoamuliwa zamani za kale,ⁱ haikawii, na maangamizi yao hayalali.^j

4 Hakika Mungu hakujizua kuwaadhibu malaika waliofanya dhambi,^k bali aliwatupa ndani ya Tartaro,^{*l} akiwaweka kwenye minyororo[#] ya giza

1:21 *Tnn., "walivyochukuliwa." 2:2 *Au "ufidhuli; matendo yao ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki, *a-sel/gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:4, 8, 9 *Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:4 *Au labda, "mashimo."

SURA YA 1

a Zb 119:105
Yoh 1:9

b Hes 24:17
Ufu 22:16

c 2Ti 3:16

d 2Sa 23:2
Mdo 1:16
Mdo 28:25
1Pe 1:11

SURA YA 2

e Mt 24:24
1Ti 4:1

f 1Ko 6:20

g Yud 4

h Isa 52:5

i Yud 4

j 2Pe 3:9

k Mwa 6:4
Efe 6:12

l 1Pe 3:19, 20

Safu ya 2

a Yud 6

b Mwa 7:23

c Mwa 6:9
Ebr 11:7

d Mwa 8:18

e 2Pe 3:6

f Mwa 19:24, 25

g Yud 7

h Mwa 19:15, 16

i Zb 34:19
1Ko 10:13
2Ti 4:18
Ufu 3:10

j Ro 2:5
2Pe 3:7

k Yud 7

l Kut 22:28
Yud 8

m Yud 9

zito ili wawekwe akiba kwa ajili ya hukumu.^a **5** Naye hakujizua kuuadhibu ulimwengu wa kale,^b bali alimlinda salama Noa, mhubiri wa uadilifu,^c pamoja na wengine saba^d alipoleta gharika juu ya ulimwengu wa watu wasiomwogopa Mungu.^e **6** Na kwa kuyageuza majiji ya Sodom na Gomora kuwa majivu, aliyahukumu^f akiweka kielelezo kwa watu wasiomwogopa Mungu kuhusu mambo yatakayokuja.^g **7** Naye alimwokoia Loti mwadilifu,^h aliyetaabishwa sana na mwene-ndo mpotovu* wa waasi sheria— **8** kwa maana siku baada ya siku mtu huyo mwadilifu alikuwa akiitasa nafsi* yake yenye uadilifu kwa sababu ya matendo ya kuasi sheria aliyoonna na kusikia alipokuwa akiishi miongoni mwao. **9** Hivyo basi, Yehova[#] anajua jinsi ya kuwakomboa kutoka kwenye jaribu watu wenye ujitoaji-kimungu,^{*i} lakini kuwaweka akiba watu wasio waadilifu ili waangamizwe^Δ katika siku ya hukumu,^j **10** hasa wale wanaotaka kutia unajisi miili ya wengine^k na ambao hudharau mamlaka.^l

Wana ujasiri na ushupavu, hawaogopi kuwatukana watukufu, **11** lakini malaika, ingawa ni wakuu zaidi katika nguvu na uwezo, hawawashitaki kwa matukano, kwa sababu wanamheshimu* Yehova.^{#m} **12** Lakini watu hawa,

2:7 *Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki, *a-sel/gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:9, 11 *Angalia Nyongeza A5. 2:9 ^ΔTnn., "wakatiliwe mbali." 2:11 *Au "wana heshima mbele za."

kama wanyama wanaotenda kwa silika na wanaozaliwa* ili kukamatwa na kuangamizwa, wanayatukana mambo wasioyajua.^a Watapata maangamizo yanayoletwa na mwendo wao wenyewe wa maangamizi, **13** wakipata madhara kama thawabu ya mwendo wao wenyewe madhara.

Wanafurahia kuishi maisha ya anasa,^b hata mchana. Wao ni madoa na dosari, wanafurahia* mafundisho yao ya udanganyifu huku wakila karamu pamoja nanyi.^c **14** Macho yao yamejaa uzinzi^d na hawawezi kuachana na dhambi, nao huwashawishi wasio imara.* Moyo wao umezoezwa kuwa na pupa. Wao ni watoto waliolaaniwa. **15** Wameiacha njia iliyonyooka, wamepotoshwa. Wameifuata njia ya Balaamu^e mwana wa Beori, aliyependa thawabu ya kuteinda makosa,^f **16** lakini akakaripiwa kwa sababu hakuifanya yaliyo sawa.^g Mnyama wa kubeba mizigo asiye na sauti alizungumza kwa sauti ya mwanadamu na kuzuia mwendo wa kiwazimu wa nabii huyo.^h

17 Hao ni chemchemi zizi na maji na ukungu unao sukumwa na dhoruba kali, nao wamewekewa akiba giza zito kabisa.ⁱ **18** Wao husema maneno ya kujigamba yasiyo na maana. Kwa kuvutia tamaa za mwili^j na kwa matendo ya upotovu wa maadili,* wa-

2:12 *Au "wanazaliwa kiasili." 2:13

*Au "wanaojifurahisha bila kujizuia katika." 2:14 *Au "nafsi zisizo imara."

2:18 *Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki, *a-sef'ge'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 2

a Yud 10

b Ro 13:13

c Yud 12

d Mt 5:28

e Hes 22:5, 6
Yud 11
Ufu 2:14f Hes 22:7
Ne 13:2g Hes 22:31, 34
Hes 31:8

h Hes 22:28

i Yud 12, 13

j Yud 16

Safu ya 2

a 2Pe 2:14

b 1Pe 2:16

c Ro 6:16

d 2Pe 1:4

e Ebr 6:4-6
Ebr 10:26f Lu 12:47
Yoh 15:22

g Met 26:11

SURA YA 3

h Ro 15:15
2Pe 1:13

i Yud 17, 18

j Yer 17:15
Mt 24:48
Lu 12:45

nawashawishi watu waliotoka tu kuponyoka kutoka kwa watu wanaoishi katika kosa.^a

19 Wanawaahidi uhuru, huku wao wenyewe wakiwa watumwa wa uharibifu;^b kwa maana yeyote anayeshindwa na mwingine, ni mtumwa wake.*^c

20 Hakika ikiwa baada ya kuponyoka unajisi wa ulimwengu^d kupitia ujuzi sahihi kumhusu Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, wanajiingiza tena katika mambo haya na kushindwa, mwisho wao unakuwa mbaya zaidi kuliko mwanzo wao.^e **21** Ingekuwa afadhali kwao kama hawangejua kwa usahihi njia ya uadilifu kuliko baada ya kuijua wageuke kutoka kwenye amri takatifu waliyopokea.^f **22** Wamepatwa na ukweli wa methali inayosema: "Mbwa ameyarudia mata-pishi yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa kwenye matope."^g

3 Wapendwa, sasa hii ndiyo barua ya pili ninayowaa-ndikia, ambayo kama katika barua yangu ya kwanza, ninachochea uwezo wenu wa kifikiri vizuri kwa kuwakumbusha,^h **2** ili mkumbuke maneno yaliyosemwa hapo mwanzoni* na manabii watakatifu na amri ya Bwana na Mwokozi kupitia mitume wenu. **3** Kwanza kabisa mjue kwamba katika siku za mwisho wadhihakiki watakuja na dhihaka zao, wakitenda kulingana na tamaa zao wenyewe.ⁱ **4** na kusema: "Kuko wapi huko kuwapo kwake kulikoahidiwa?^j Kwani tangu siku mababu

2:19 *Au "anayeshindwa na kitu fulani, ni mtumwa wa kitu hicho." 3:2 *Au "mambo yaliyotabiriwa."

zetu walipolala usingizi katika kifo, mambo yote yanaendelea kama yalivyokuwa tangu mwanzo wa uumbaji.”^a

5 Kwa maana, wanapuuzwa kimakusudi jambo hili, kwamba zamani za kale kulikuwa na mbingu na dunia iliyokuwa imesimama imara kutoka katika maji na katikati ya maji kwa neno la Mungu;^b **6** na kwamba kwa njia hizo ulimwengu wa wakati huo uliangamia kwa ghariba ya maji.^c **7** Lakini kwa neno hilo, mbingu na dunia zilizopo sasa zimewekwa akiba kwa ajili ya moto na zinawekwa mpaka siku ya hukumu na ya kuangamizwa kwa watu wasiomwogopa Mungu.^d

8 Hata hivyo, wapendwa, msikose kujua jambo hili, kwamba siku moja kwa Yehova* ni kama miaka elfu na miaka elfu ni kama siku moja.^e

9 Yehova* hakawii kuhusiana na ahadi yake,^f kama watu fulani wanavyodhani,^g bali ni mwenye subira kwenu kwa sababu hataki yeyote aangamizwe bali hutaka wote wafiki toba.^g **10** Lakini siku ya Yehova*^h itakuja kama mwi-zi,ⁱ siku ambayo mbingu zitapitilia mbali^j kwa mngurumo,^g lakini vitu vyake vya msingi vikiwa moto sana vitayeyushwa, na dunia na kazi zilizo ndani yake zitafunuliwa.^k

11 Kwa kuwa vitu hivyo vyote vitayeyushwa kwa njia hiyo, fikirieni mnapaswa kuwa watu wa aina gani katika matendo matakatiifu ya mwe-

3:8-10, 12 *Angalia Nyongeza A5. **3:9** *Au “wanavyoona kukawia.” **3:10** *Au “sauti ya kuvuma.”

SURA YA 3

a Eze 12:22, 27

b Mwa 1:6, 9

c Mwa 7:11, 23
Mt 24:38, 39d Kum 7:10
2Th 1:7-9

e Zb 90:4

f Hab 2:3

g Ro 2:4

h Yoe 2:31
Sef 1:14

i 1Th 5:2

j Ufu 21:1

k Zb 37:10
Isa 13:9
Sef 1:18
Ufu 6:14

Safu ya 2

a Sef 1:14

b Isa 34:4

c Isa 65:17
Isa 66:22
Ufu 21:1

d Isa 11:4, 5

e 2Ko 13:11

f Ro 2:4

g Mt 24:24
Efe 4:14

nendo na vitendo vya ujitoajikimungu,* **12** huku mkisubiri na kuweka karibu akilini[#] kuwapo kwa siku ya Yehova,*^a siku ambayo mbingu zitateketezwa^b kwa moto na vitu vya msingi vitayeyuka kwa joto kali! **13** Lakini kulingana na ahadi yake tunangojea mbingu mpya na dunia mpya,^c na humo uadilifu utakaa.^d

14 Kwa hiyo, wapendwa, kwa kuwa mnangojea mambo hayo, fanyeni yote mnayoweza ili mwishowe awapate mkiwa bila doa wala dosari na mkiwa katika amani.^e **15** Zaidi ya hayo, ioneni subira ya Bwana wetu kuwa wokovu, kama ndugu yetu mpendwa Paulo alivyowaandikia pia kulingana na hekima aliyopewa,^f **16** akizunguma kuhusu mambo hayo kama anavyofanya katika barua zake zote. Hata hivyo, ni vigumu kuyaelewa mambo fulani katika barua hizo, na watu wasio na ujuzi* na wasio imara wanayapotisha, kama wanavyoyafanya Maandiko mengine pia, kwa maangamizi yao wenyewe.

17 Kwa hiyo, wapendwa, kwa kuwa mmpata ujuzi huu mapema, jilindeni ili msipotoshwe pamoja nao kwa kosa la waasi sheria, na kuanguka kutoka kwenye msimamo wenu imara.*^g **18** Hapana, bali endeleeni kukua katika fadhili zisizostahiliwa na ujuzi kumhusu Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Na awe na utukufu sasa na mpaka siku ya umilele. Amina.

3:11 *Angalia Kamusi, uku. 2012. **3:12** *Au “kutamani sana.” Tnn., “kuharakisha.” **3:16** *Au “ambao hawajafundishwa.” **3:17** *Au “thabiti.”

BARUA YA KWANZA YA
YOHANA

YALIYOMO

- | | |
|--|--|
| <p>1 Neno la uzima (1-4)
 Kutembea katika nuru (5-7)
 Uhitaji wa kuungama dhambi (8-10)</p> <p>2 Yesu, dhabihu ya upatanisho (1, 2)
 Kushika amri zake (3-11)
 Amri ya zamani na amri mpya (7, 8)
 Sababu za kuandika (12-14)
 Msiupende ulimwengu (15-17)
 Onyo dhidi ya mpinga-Kristo (18-29)</p> <p>3 Sisi ni watoto wa Mungu (1-3)
 Tofauti kati ya watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi (4-12)
 Yesu atazivunja kazi za Ibilisi (8)
 Mpendane (13-18)</p> | <p>Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu (19-24)</p> <p>4 Kuyajaribu maneno yaliyoongozwa na roho (1-6)
 Kumjua na kumpenda Mungu (7-21)
 “Mungu ni upendo” (8, 16)
 Hakuna woga katika upendo (18)</p> <p>5 Kumwamini Yesu huushinda ulimwengu (1-12)
 Maana ya kumpenda Mungu (3)
 Uhakika katika nguvu za sala (13-17)
 Jihadharini katika ulimwengu mwovu (18-21)
 Ulimwengu mzima katika nguvu za yule mwovu (19)</p> |
|--|--|

1 Kile kilichokuwapo tangu mwanzo, tulichokisia na kukiona kwa macho yetu, ambacho tumekitazama na mikono yetu ikakigusa, kuhusiana na neno la uzima,^a **2** (ndiyo, uzima ulifunuliwa, nasi tumeona na tunatoa ushahidi^b na kuwajulisha kuhusu uzima wa milele^c ambao Baba alikuwa nao, na uliofunuliwa kwetu), **3** kile ambacho tumeona na kusikia tunawajulisha pia,^d ili ninyi vilevile muwe na ushirika pamoja nasi. Na huu ushirika wetu ni pamoja na Baba na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.^e **4** Nasi tunaandika mambo haya ili shangwe yetu iwe kamili.

5 Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka kwake nasi tunawatangazia ninyi: Mungu ni nuru,^f na hakuna giza kamwe

SURA YA 1

- a Yoh 1:4
 Yoh 6:68
- b Yoh 21:24
 Mdo 2:32
- c Yoh 17:3
- d Yoh 15:26, 27
 Mdo 4:20
- e Yoh 17:20, 21
- f Yak 1:17

Safu ya 2

- a 2Ko 6:14
 Efe 5:8
 Tit 1:16
 1Yo 2:4
- b Ro 3:25
 Efe 1:7
 Ebr 9:14
 Ebr 10:22
 Ufu 1:5
- c 1Fa 8:46
 Mhu 7:20
- d Zb 32:5
 Met 28:13
 Yak 5:16

ndani yake.* **6** Ikiwa tuna-sema, “Tuna ushirika pamoja naye,” na bado tunaendelea kutembea katika giza, tunasema uwongo nasi hatuishi kulingana na kweli.^a **7** Hata hivyo, ikiwa tunatembea katika nuru kama yeye mwenyewe alivyo katika nuru, tuna ushirika sisi kwa sisi, na damu ya Yesu Mwana wake hutusafisha kutoka katika dhambi yote.^b

8 Ikiwa tunasema, “Hatuna dhambi,” tunajipotosha wenyewe^c na kweli haimo ndani yetu. **9** Tukiungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na mwadilifu naye atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha ukosefu wote wa uadilifu.^d **10** Ikiwa tunasema, “Hatujatenda dhambi,” tunamfanya yeye kuwa mwongo, na neno lake halimo ndani yetu.

1:5 *Au “katika muungano naye.”

2 Watoto wangu wadogo, ninawaandikia mambo haya ili msitende dhambi. Na bado, yeyote akitenda dhambi, tuna msaidizi* kwa Baba, Yesu Kristo,^a mtu mwadilifu.^b **2** Naye ni dhabihu ya upatanisho*^c kwa ajili ya dhambi zetu,^d lakini si kwa ajili ya dhambi zetu tu bali pia dhambi za ulimwengu wote.^e **3** Na kwa jambo hili tunatambua kwamba tumemjua yeye, yaani, tukiendelea kuzishika amri zake. **4** Mtu anayesema, "Mimi nimemjua," na bado hashiki amri zake ni mwongo, na kweli haimo ndani ya mtu huyo. **5** Lakini yeyote anayeshika neno lake, kwa kweli upendo wa Mungu umekamilishwa katika mtu huyo.^f Hivyo ndivyo tunajua kwamba sisi tumo katika muungano na yeye.^g **6** Mtu anayesema kwamba anaka katika muungano na yeye, ana wajibu wa kuendelea kutembea kama huyo alivyotembea.^h

7 Wapendwa, siwaandikii amri mpya, bali amri ya zamani ambayo mmekuwa nayo tangu mwanzo.ⁱ Amri hiyo ya zamani ni neno ambalo mlisikia. **8** Tena, ninawaandikia amri mpya, ambayo ni ya kweli kumhusu yeye na kuwahusu ninyi, kwa sababu giza linapitilia mbali na nuru ya kweli tayari inaangaza.^j

9 Mtu anayesema kwamba yumo katika nuru na bado anamchukia^k ndugu yake bado yumo katika giza.^l **10** Mtu anayempenda ndugu yake hukaa katika nuru,^m naye hana kikwazo chochote. **11** La-

2:1 *Au "wakili." 2:2 *Au "dhabihu ya kufunika dhambi; njia ya kuleta maelewano."

SURA YA 2

a Ro 8:34

Ebr 7:25

b 1Ti 2:5

c 1Ko 5:7

d Isa 53:5

Ro 3:25

1Ti 1:15

Ebr 2:17

1Pe 2:24

1Yo 4:10

e Mt 20:28

Yoh 1:29

f 1Yo 4:18

g Yoh 14:20

Yoh 17:21

h Yoh 13:15

1Pe 2:21

i Yoh 13:34

2Yo 5

j Yoh 1:9

Yoh 8:12

k Efe 4:31

Kol 3:8

l 1Ko 13:2

1Yo 3:15

m Efe 5:8

Safu ya 2

a 1Yo 4:20

b Yoh 12:35

c Lu 24:47

Mdo 4:12

Mdo 10:43

d Yak 4:7

1Yo 5:19

Ufu 12:10, 11

e Yoh 17:25

f Efe 6:10

g 3Yo 3

h Ro 8:37

i Ro 12:2

1Ko 7:31

Tit 2:11, 12

j Mt 6:24

Yak 4:4

k Mt 5:28

Ro 13:14

l Mwa 3:6

Met 27:20

Mt 4:8

m 1Ko 7:31

1Pe 1:24

n Zb 37:29

Mt 7:21

Yoh 6:40

o 2Th 2:3

2Pe 2:1

p 2Th 2:7

2Yo 7

Yud 4

kini mtu anayemchukia ndugu yake yumo katika giza na anatembea katika giza,^a naye hajui anakoenda,^b kwa sababu giza limeyapofusha macho yake.

12 Ninawaandikia ninyi watoto wadogo, kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu kwa ajili ya jina lake.^c **13** Ninawaandikia ninyi akina baba, kwa sababu mmemjua yule aliye wa tangu mwanzo. Ninawaandikia ninyi vijana, kwa sababu mmemshinda yule mwovu.^d Ninawaandikia ninyi watoto wadogo, kwa sababu mmemjua Baba.^e

14 Ninawaandikia ninyi akina baba, kwa sababu mmemjua yule aliye wa tangu mwanzo. Ninawaandikia ninyi vijana, kwa sababu mna nguvu^f na neno la Mungu hukaa ndani yenu^g nanyi mmemshinda yule mwovu.^h

15 Msiupende ulimwengu au vitu vilivyo katika ulimwengu.ⁱ Yeyote akiupenda ulimwengu, kumpenda Baba hakumo ndani yake;^j **16** kwa sababu kila kitu katika ulimwengu—tamaa ya mwili^k na tamaa ya macho^l na mtu kujionyesha mali zake maitshani*—hakitokani na Baba, bali hutokana na ulimwengu. **17** Zaidi ya hayo, ulimwengu unapitilia mbali na pia tamaa yake,^m lakini yule anayefanya mapenzi ya Mungu anadamu milele.ⁿ

18 Watoto wadogo, ni saa ya mwisho, na kama vile mlivyo-sikia kwamba mpinga-Kristo anakuja,^o hata sasa wapinga-Kristo wengi wametokea,^p na kwa sababu hiyo tuna-

2:16 *Au "mtu kujigamba kuhusu mali zake."

jua kwamba ni saa ya mwisho. **19** Waliondoka miongoni mwetu, lakini hawakuwa wa namna yetu,*^a kwa maana kama wangukuwa wa namna yetu, wangebaki pamoja nasi. Lakini waliondoka ili ionekane kwamba si wote walio wa namna yetu.^b **20** Nanyi mmetiwa mafuta kutoka kwa yule mtakatifu,^c na nyote mna ujuzi. **21** Ninawaandikia, si kwa sababu hamwijui kweli,^d bali kwa sababu mnaijua, na kwa sababu hakuna uwongo unaotokana na kweli.^e

22 Ni nani aliye mwongo kama si yule anayekana kwamba Yesu ndiye Kristo?^f Huyo ndiye mpinga-Kristo,^g yule anayemkana Baba na Mwana. **23** Kila mtu anayemkana Mwana hana Baba pia,^h bali yeyote anayemkiri Mwanaⁱ ana Baba pia.^j **24** Lakini mambo mliyosikia tangu mwanzo yanapaswa ku-kaa ndani yenu.^k Ikiwa mambo mliyosikia tangu mwanzo yanakaa ndani yenu, ninyi pia mtakaa katika muungano na Mwana na katika muungano na Baba. **25** Zaidi ya hayo, hili ndilo jambo alilotuahidi yeye mwenyewe, uzima wa milele.^l

26 Ninawaandikia mambo haya kuhusu wale wanaojaribu kuwapotosha ninyi. **27** Kutiwa mafuta ambako mlipokea kutoka kwake^m hukaa ndani yenu, na hamhitaji kufundishwa na yeyote; lakini kutiwa mafuta kutoka kwake kunawafundisha kuhusu mambo yote,ⁿ na ni kweli si uwongo. Kama kulivyowafundisha ninyi, kaeni katika muungano na

SURA YA 2

a Mdo 20:30

b 1Ko 11:19

c 2Ko 1:21
1Yo 2:27

d Yoh 8:31, 32

e Yoh 8:44

f 1Yo 4:3
2Yo 7

g 1Yo 2:18

h Yoh 5:23
2Yo 9

i Ro 10:9, 10

j 1Yo 4:15

k Yoh 14:23
2Yo 6l Yoh 17:3
1Yo 1:2m 2Ko 1:21
1Yo 2:20n Yoh 14:26
Yoh 16:13

Safu ya 2

a Yoh 17:21

b 1Yo 4:17

c 1Pe 1:23
1Yo 4:7

SURA YA 3

d Yoh 3:16

e Yoh 1:12, 13

f Yoh 15:19

g Yoh 17:25

h Ro 8:15, 16
Efe 1:5i 1Ko 15:49
Flp 3:20, 21

j 2Ko 7:1

k Law 16:21, 22
Isa 53:11
Yoh 1:29

l Ro 6:12

m Mwa 3:14
Yoh 8:44

yeye.^a **28** Basi sasa, watoto wadogo, kaeni katika muungano na yeye, ili atakapofunuliwa tuwe na uhuru wa kusema^b bali tusiaibike wakati wa kuwapo kwake. **29** Ikiwa mnajua yeye ni mwadilifu, mna-jua pia kwamba kila mtu aliye na mazoea ya kufanya uadilifu amezaliwa kutokana naye.^c

3 Oneni upendo ambao Baba ametuonyesha,^d kwamba tunapaswa kuitwa watoto wa Mungu!^e Na hivyo ndivyo tulivyo. Ndiyo sababu ulimwengu hautujui,^f kwa sababu haumjui yeye.^g **2** Wapendwa, sasa sisi ni watoto wa Mungu,^h lakini bado haijafunuliwa jinsi tutakavyokuwa.ⁱ Tunajua kwamba atakapofunuliwa tutakuwa kama yeye, kwa sababu tutamwona kama alivyo. **3** Na kila mtu aliye na tumaini hili ndani yake hujisafisha,^j kama huyo alivyo safi.

4 Kila mtu aliye na mazoea ya kufanya dhambi anaendelea pia kufanya uasi sheria, na dhambi ni uasi sheria. **5** Mnajua pia kwamba alifunuliwa ili kuondoa dhambi zetu,^k na hakuna dhambi ndani yake. **6** Kila mtu anayekaa katika muungano na yeye hana mazoea ya kufanya dhambi; mtu yeyote aliye na mazoea ya kufanya dhambi hajamwona wala kumjua. **7** Watoto wadogo, yeyote asiwapotoshe; mtu anayeendelea kufanya uadilifu ni mwadilifu, kama huyo alivyo mwadilifu. **8** Mtu aliye na mazoea ya kufanya dhambi hutokana na Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akifanya dhambi tangu mwanzo.^m Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu

alifunuliwa, ili avunje* kazi za Ibilisi.^a

9 Kila mtu ambaye amezaliwa kutokana na Mungu haendelei kufanya dhambi,^b kwa sababu mbegu* Yake hukaa ndani ya mtu huyo, naye hawazi kuendelea kufanya dhambi, kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.^c **10** Watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi ni wazi kwa jambo hili: Yeyote ambaye haendelei kufanya uadilifu hatokani na Mungu, wala yule ambaye hampendi ndugu yake.^d **11** Kwa maana huu ndio ujumbe ambao mmesikia tangu mwanzo, kwamba tunapaswa kupendana;^e **12** si kama Kaini, aliyetokana na yule mwovu akamuua ndugu yake. Na kwa nini alimuua?^f Kwa sababu matendo yake mwenyewe yalikuwa maovu,^g lakini matendo ya ndugu yake yalikuwa ya uadilifu.^h

13 Akina ndugu, msishangae kwamba ulimwengu unawachukia.ⁱ **14** Tunajua kwamba tumevuka kutoka kifo mpaka uzima,^j kwa sababu tunawapenda akina ndugu.^k Mtu ambaye hapendi hukaa katika kifo.^l **15** Kila mtu anayemchukia ndugu yake ni muuaji,^m nanyi mnajua kwamba hakuna muuaji aliye na uzima wa milele ndani yake.ⁿ **16** Sisi tumejua upendo, kwa sababu huyo alitoa uhai wake* kwa ajili yetu,^o nasi tuna wajibu wa kutoa uhai wetu[#] kwa ajili ya ndugu zetu.^p **17** Lakini yeyote aliye na mali za ulimwengu huu akimwona ndu-

3:8 *Au "aangamize." 3:9 *Yaani, mbegu inayoweza kuzaa, au inayotokeza matunda. 3:16 *Au "nafsi yake." #Au "nafsi zetu."

SURA YA 3

- a Yoh 16:33
Ebr 2:14
b 1Yo 5:18
c 1Pe 1:23
d 1Yo 4:8
e Yoh 13:34
1Yo 2:7
2Yo 5
f Mwa 4:8
g Mwa 4:5
h Mwa 4:4
Ebr 11:4
i Mt 5:11
Yoh 15:18
2Ti 3:12
j Yoh 5:24
Ro 8:2
k 1Yo 2:10
l Yoh 3:36
m Mt 5:21, 22
Efe 4:31
n Mwa 9:6
Hes 35:31
Ufu 21:8
o Yoh 3:16
Yoh 13:1
Yoh 15:13
p Yoh 13:15
Ro 16:3, 4
1Th 2:8

Safu ya 2

- a Kum 15:7, 8
Lu 3:11
Ro 12:13
Yak 2:15, 16
1Yo 4:20
b Ro 12:9
c Yak 1:22
Yak 2:17
d 1Pe 1:22
e Ebr 4:13
f Ebr 4:16
1Yo 5:14
g Zb 34:15
Mt 7:8
1Pe 3:12
h Yoh 6:29
i Yoh 13:34
j 1Yo 2:24
k Yoh 14:23

SURA YA 4

- l 2Th 2:1, 2
1Ti 4:1
m Ufu 22:6
n 2Pe 2:1

gu yake akiwa na uhitaji naye akatae kumhurumia, anawezaje kuwa na upendo wa Mungu ndani yake?^a **18** Watoto wadogo, tunapaswa kupendana, si kwa neno au kwa ulimi,^b bali kwa tendo^c na kweli.^d

19 Kwa jambo hili tutajua kwamba tunatokana na kweli, nasi tutaihakikishia* mioyo yetu mbele zake **20** kuhusu jambo lolote ambalo huenda mioyo yetu ikatuhukumu, kwa sababu Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua mambo yote.^e **21** Wapendwa, ikiwa mioyo yetu hai-tuhukumu, tuna uhuru wa kusema na Mungu;^f **22** na chochote tunachoomba tunapokea kutoka kwake,^g kwa sababu tunazishika amri zake na tunafanya mambo yanayopendeza machoni pake. **23** Kwa kweli, hii ndiyo amri yake: kwamba tuwe na imani katika jina la Mwana wake Yesu Kristo^h na tupendane,ⁱ kama vile alivyotupatia amri. **24** Zaidi ya hayo, mtu anayeshika amri zake hukaa katika muungano na yeye, na yeye katika muungano na mtu huyo.^j Na kupitia roho aliyotupatia, tunajua kwamba ana-kaa katika muungano pamoja nasi.^k

4 Wapendwa, msiamini kila neno lililoongozwa na roho,^l lakini yajaribuni maneno yaliyoongozwa na roho ili kuona kama yanatoka kwa Mungu,^m kwa kuwa manabii wengi wa uwongo wameingia ulimwenguni.ⁿ

2 Hivi ndivyo mnavyojua ikiwa neno lililoongozwa na

3:19 *Au "tutaishawishi; tutaisadikisha." 4:1 *Tnn., "kila roho."

roho limetoka kwa Mungu: Kila neno lililoongozwa na roho linalokiri kwamba Yesu Kristo alikuja katika mwili lina-
toka kwa Mungu.^a **3** Lakini kila neno lililoongozwa na roho ambalo halimkiri Yesu halitoki kwa Mungu.^b Zaidi ya hayo, hili ndilo neno lililoongozwa na roho la yule mpinga-Kristo ambalo mmesikia kwamba linakuja,^c na sasa tayari limo ulimwenguni.^d

4 Ninyi mnatokana na Mungu, watoto wadogo, nanyi mmewashinda,^e kwa sababu yule aliye katika muungano na ninyi^f ni mkuu kuliko yule aliye katika muungano na ulimwengu.^g **5** Wao hutokana na ulimwengu,^h ndiyo sababu wanasema mambo yanayotokana na ulimwengu na ulimwengu huwasikiliza.ⁱ **6** Sisi tunatokana na Mungu. Yeyote anayemjua Mungu hutusikiliza,^j yeyote ambaye hatokani na Mungu hatusikilizi.^k Hivi ndivyo tunavyolito-fautisha neno la kweli lililoongozwa na roho na neno lenye kosa lililoongozwa na roho.^l

7 Wapendwa, na tuendeele kupendana,^m kwa sababu upendo unatoka kwa Mungu, na kila mtu ambaye hupenda amezaliwa kutokana na Mungu na anamjua Mungu.ⁿ **8** Yeyote ambaye hapendi hajamjua Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo.^o **9** Hivi ndivyo upendo wa Mungu ulivyofunuliwa kwetu, kwamba Mungu alimtuma Mwana wake mzaliwa-pekee^p ulimwenguni ili tupate uzima kupitia yeye.^q **10** Hivi ndivyo upendo ulivyo, si kwamba sisi tumempenda Mungu,

SURA YA 4

a Yoh 1:14
1Ko 12:3
Ufu 19:10

b 1Yo 2:22

c 2Th 2:7
1Yo 2:18

d Mdo 20:29, 30

e 1Yo 5:4

f Yoh 17:21

g Efe 2:2

h 1Yo 5:19

i Yoh 15:19

j Yoh 10:27

k Yoh 8:47

l 1Yo 4:1

m 1Pe 1:22

n 1Yo 4:16

o Kut 34:6
Mik 7:18
1Yo 4:19

p Yoh 1:14

q Yoh 3:16
Ro 5:8
Ro 8:32
1Yo 5:11

Safu ya 2

a 1Ko 5:7

b Ro 3:25
Ebr 2:17
Ebr 9:26
1Yo 2:1, 2

c Mt 18:33
Yoh 15:12
Ro 13:8
1Yo 3:16

d Kut 33:20
Yoh 1:18
Yoh 4:24
Yoh 6:46

e 1Yo 2:5

f Mt 1:21
Yoh 3:17
Yoh 12:47
Mdo 5:31

g Ro 10:9

h 1Yo 2:23, 24

i Yoh 3:16

j 1Yo 4:8

k Yoh 17:21

l Ebr 4:16
1Yo 2:28

m Ro 8:15

bali kwamba yeye alitupenda akamtuma Mwana wake kuwa dhabihu ya upatanisho*^a kwa ajili ya dhambi zetu.^b

11 Wapendwa, ikiwa Mungu alitupenda hivi, basi sisi pia tuna wajibu wa kupendana.^c

12 Hakuna mtu ambaye amemwona Mungu wakati wowote.^d Tukiendelea kupendana, Mungu hukaa ndani yetu na upendo wake unakamilishwa ndani yetu.^e **13** Hivi ndivyo tunavyojua kwamba tunakaa katika muungano na yeye na yeye katika muungano na sisi, kwa sababu ametupatia roho yake. **14** Isitoshе, sisi wenyewe tumemwona na tunatoa ushahidi kwamba Baba amemtuma Mwana wake kuwa mwokozi wa ulimwengu.^f **15** Yeyote anayekiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu,^g Mungu hukaa katika muungano na mtu huyo na yeye katika muungano na Mungu.^h **16** Nasi tumejua na tumeamini kwamba Mungu anatupenda.ⁱ

Mungu ni upendo,^j na mtu anayekaa katika upendo hukaa katika muungano na Mungu, na Mungu hukaa katika muungano na yeye.^k **17** Kwa njia hii upendo umekamilishwa ndani yetu, ili tuwe na uhuru wa kusema*^l katika siku ya hukumu, kwa sababu, kama huyo alivyo, ndivyo tulivyo katika ulimwengu huu. **18** Hakuna woga katika upendo,^m lakini upendo mkamilifu hutupa* woga nje, kwa sababu woga hutuzuia. Kwa

4:10 *Au "dhabihu kwa ajili ya kufunika; njia ya kuleta maelewano." **4:17** *Au "tuwe na uhakika." **4:18** *Au "husukuma."

kweli, mtu aliye mwoga haja-kamilishwa katika upendo.^a **19** Sisi tuna upendo, kwa sababu alitupenda kwanza.^b

20 Yeyote akisema, "Nina-mpenda Mungu," na bado ana-mchukia ndugu yake, yeye ni mwongo.^c Kwa maana mtu ambaye hampendi ndugu yake,^d ambaye amemwona, ha-wezi kumpenda Mungu ambaye hajamwona.^e **21** Nasi tuna amri hii kutoka kwake, kwamba yeyote anayempenda Mungu lazima pia ampende ndugu yake.^f

5 Kila mtu anayeamini kwa-mba Yesu ndiye Kristo amezaliwa kutokana na Mungu,^g na kila mtu anayempen-da yule aliyesababisha kuza-liwa humpenda yule ambaye amezaliwa kutokana na huyo.

2 Hivi ndivyo tunavyojua kwamba tunawapenda wato-to wa Mungu,^h kwa kumpenda Mungu na kushika amri zake.

3 Kwa maana kumpenda Mungu humaanisha hivi, kwa-mba tuzishike amri zake;ⁱ na bado amri zake si mzungu mzi-to,^j **4** kwa sababu kila mtu aliyezaliwa* kutokana na Mungu huushinda ulimwengu.^k Na huu ndio ushindi ambao umeushinda ulimwengu, imani yetu.^l

5 Ni nani anayeweza kuu-shinda ulimwengu?^m Ni yule anayeamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.ⁿ **6** Huyu ndiye aliyekuja kupitia maji na damu, Yesu Kristo, si kwa maji tu,^o bali kwa maji na kwa damu.^p Na roho inatoa usha-hidi,^q kwa sababu roho ndi-yo kweli. **7** Kwa maana kuna

5:4 * Tnn., "kila kitu kilichoaliwa."

SURA YA 4

- a 1Yo 2:5
b 1Yo 4:10
c 1Yo 2:4
d 1Yo 3:17
e 1Yo 4:12
f Mt 22:37, 39
Yoh 13:34
Yoh 15:12

SURA YA 5

- g Yoh 3:3
1Pe 1:3, 23
1Yo 3:9
h Yoh 1:12, 13
Ro 8:14
i Yoh 14:23
j Kum 30:11
Mik 6:8
k Yoh 16:33
1Yo 5:18
l Efe 6:16
2Ti 4:7
Ufu 12:10, 11
m 1Yo 4:4
n Yoh 20:31
o Mt 3:13
p Mdo 20:28
Efe 1:7
1Pe 1:19
q Mt 3:16
Yoh 1:32, 33

Safu ya 2

- a Lu 3:22
Lu 4:18
b Lu 3:21
c Ebr 9:14
d Yoh 3:33
e Yoh 17:3
f Yoh 5:26
g Yoh 3:36
h Yoh 20:31
i 1Yo 1:2
j Ebr 4:16
1Yo 3:21
k Met 15:29
l Lu 11:13
Yoh 14:13
m Yak 5:15
1Yo 1:9
n Mt 12:31
Mk 3:29
Lu 12:10
Ebr 6:4-6
Ebr 10:26

vitu vitatu vinavyotoa usha-hidi: **8** roho^a na maji^b na damu;^c na hivyo vitatu vina-kubaliana.

9 Tukikubali ushahidi wa wanadamu, ushahidi wa Mungu ni mkuu zaidi. Kwa sababu huu ndio ushahidi ambao Mungu hutoa, ushahidi ambao ametoa kumhusu Mwana wake. **10** Mtu anayemwamini Mwana wa Mungu, ana ushahi-di ndani yake. Mtu asiyemwa-mini Mungu amemfanya yeye kuwa mwongo,^d kwa sababu hana imani katika ushahidi uliotolewa na Mungu kumhu-su Mwana wake. **11** Na huu ndio ushahidi, kwamba Mungu alitupatia uzima wa mile-le,^e na uzima huu umo ndani ya Mwana wake.^f **12** Mtu ali-ye na Mwana ana uzima huu; mtu ambaye hana Mwana wa Mungu hana uzima huu.^g

13 Ninawaandikia mambo haya ili ninyi mlio na imani ka-tika jina la Mwana wa Mungu^h mjue kwamba mna uzima wa milele.ⁱ **14** Na huu ndio uha-kika tulio nao kwake,^j kwamba tukiomba chochote kulinga-na na mapenzi yake, yeye hu-tusikia.^k **15** Na ikiwa tunajua kwamba anatusikia kuhusiana na chochote tunachoomba, tunajua kwamba tutapata mambo tuliyomwomba, kwa kuwa tumeyaomba kwake.^l

16 Yeyote akimwona ndugu yake akifanya dhambi isi-yoleta kifo, yeye ataomba, na Mungu atampa huyo uzima,^m ndiyo, kwa wale ambao hawa-fanyi dhambi inayoleta kifo. Kuna dhambi ambayo huleta kifo.ⁿ Simwambii aombe ku-husu dhambi hiyo. **17** Uko-sefu wote wa uadilifu ni dha-

mbi,^a na bado kuna dhambi isiyoleta kifo.

18 Tunajua kwamba kila mtu aliyezaliwa kutokana na Mungu hana mazoea ya kufanya dhambi, lakini yeye hulindwa na yule aliyezaliwa kutokana na Mungu,^{*} na yule mwovu hawezi kumshika.^{#b} **19** Tunajua tunatokana na Mungu, lakini ulimwengu mzima unakaa katika nguvu za

5:18 *Yaani, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. #Au "hamshiki imara."

SURA YA 5

a 1Yo 3:4

b Yoh 17:15

Safu ya 2

a Mt 13:19

Lu 4:6

Yoh 12:31

b 1Ti 3:16

c Yoh 17:20, 21

d Yoh 17:3

e 1Ko 10:14

yule mwovu.^a **20** Hata hivyo, tunajua kwamba Mwana wa Mungu amekuja,^b naye ametupatia ufahamu* ili tuweze kumjua yule aliye wa kweli. Nasi tumo katika muungano na yule aliye wa kweli,^c kupitia Mwana wake, Yesu Kristo. Huyo ndiye Mungu wa kweli na uzima wa milele.^d **21** Watoto wadogo, jiepusheni na sanamu.^e

5:20 *Tnn., "uwezo wa kufikiri; uwezo wa akili."

BARUA YA PILI YA

YOHANA

YALIYOMO

Salamu (1-3)

Endeleeni kutembea katika kweli (4-6)

Jihadharini na wadanganyifu (7-11)

Msiwasalimu (10, 11)

Mipango ya kuwatembelea na salamu (12, 13)

1 Mwanamume mzee,^{*} kwa bibi aliyechaguliwa na kwa watoto wake, ambao ninawapenda kweli, na si mimi tu, bali pia wale wote ambao wamejua kweli, **2** kwa sababu ya kweli inayokaa ndani yetu na itakayokuwa pamoja nasi milele. **3** Tutakuwa na fadhili zisizostahiliwa, rehema, na amani kutoka kwa Mungu Baba na kutoka kwa Yesu Kristo, Mwana wa Baba, pamoja na kweli na upendo.

4 Ninashangilia sana kwa sababu nimekuta baadhi ya

1 *Au "Mzee."

Safu ya 2

a 2Ko 4:2

3Yo 3

b Yoh 13:34

Yoh 15:12

1Pe 4:8

1Yo 2:7

c Yoh 14:21

1Yo 2:5

d Mt 7:15

Mdo 20:29, 30

2Th 2:3, 7

2Pe 2:1

Ufu 2:2

e 1Yo 4:2

watoto wako wakitembea katika kweli,^a kama tulivyopokea amri kutoka kwa Baba. **5** Bibi, sasa ninakuomba kwamba tupendane. (Siwaandikii amri mpya, bali amri tuliyokuwa nayo tangu mwanzo.)^b **6** Na upendo unamaanisha hivi, kwamba tuendelee kutembea kulingana na amri zake.^c Hii ndiyo amri, kama mlivyosikia tangu mwanzo, kwamba mnapaswa kuendelea kutembea ndani yake. **7** Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea ulimwenguni,^d wale wasiokiri kwamba Yesu Kristo alikuja katika mwili.^e

Huyu ndiye yule mdanganyifu na mpinga-Kristo.^a

8 Jihadharini, msije mkapoteza mambo ambayo tumefanya kazi ili kuyatokeza, bali mpate thawabu kamili.^b

9 Kila mtu anayevuka mipaka na ambaye hakai katika fundisho la Kristo hana Mungu.^c Mtu anayekaa katika fundisho hili ndiye aliye na Baba na Mwana pia.^d **10** Mtu yeyote akija kwenu naye haleti fundisho hili, msimpokee nyu-

a 1Yo 2:18, 22
1Yo 4:3
Yud 4

b Ebr 10:35

c Yoh 14:6
Yoh 15:6
3Yo 9

d Ebr 3:14
1Yo 2:23

Safu ya 2

a Kum 17:2-5
Ro 16:17
1Ko 5:11

mbani mwenu^a wala kumsalimu. **11** Kwa maana mtu anayemsalimu anashiriki matendo yake maovu.

12 Ingawa nina mambo mengi ya kuwaandikia, sitaki kufanya hivyo kwa karatasi na wino, bali ninatumaini kuja kwenu na kuzungumza nanyi uso kwa uso, ili shangwe yenu iwe kamili.

13 Watoto wa dada yako, yule aliyechaguliwa, wanakutumia salamu zao.

BARUA YA TATU YA YOHANA

YALIYOMO

Salamu na sala (1-4)

Gayo apongezwa (5-8)

Diotrefe aliyependa makuu (9, 10)

Demetrio ashuhudiwa vema (11, 12)

Mipango ya kutembelea na salamu (13, 14)

1 Mwanamume mzee,* kwa Gayo mpendwa, ninayempeleka kweli.

2 Mpendwa, ninasali kwa mba katika mambo yote uendelee kusitawi na kuwa na afya njema, kama unavyositawi* sasa. **3** Kwa maana nilishangilia sana akina ndugu walipokuja na kutoa ushahidi kuhusu kweli unayoshika, unapoendelea kutembea katika kweli.^a **4** Sina shangwe kubwa* kuliko hii: kwamba nisikie watoto wangu wa-

1 *Au "Mzee." 2 *Au "nafsi yako inavyositawi." 4 *Au labda, "sababu ya kushukuru."

a 2Yo 4

Safu ya 2

a 1Ko 4:15
2Ti 1:2
Tit 1:4
Flm 10

b Ebr 13:2

c Tit 3:13

d 1Ko 9:11, 12

e Mt 10:41
Flm 22
1Pe 4:9

f Ro 12:13

naendelea kutembea katika kweli.^a

5 Mpendwa, unaonyesha uaminifu kwa yale unayofanya kwa ajili ya akina ndugu, hata kama ni wageni.^b **6** Wametoa ushahidi kuhusu upelele wako mbele ya kutaniko. Tafadhali shughulikia safari yao kwa njia inayomfaa Mungu.^c **7** Kwa maana walisafiri kwa ajili ya jina lake, bila kuchukua kitu chochote^d kutoka kwa watu wa mataifa. **8** Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuwakaribisha watu kama hao,^e ili tuwe wafanyakazi wenzi katika kweli.^f

9 Niliandikia kutaniko jambo fulani, lakini Diotrefe, anayependa kuwa wa kwanza kati yao,^a hakubali kwa heshima jambo lolote kutoka kwetu.^b

10 Hiyo ndiyo sababu niki-ja, nitayashughulikia matendo anayofanya kwa kueneza maneno mabaya kutuhusu.*^c Hatosheki na hayo, bali pia anakataa kuwakaribisha kwa heshima akina ndugu;^d na wale wanaotaka kuwakaribisha, anajaribu kuwazuia na kuwataupa nje ya kutaniko.

11 Mpendwa, usiige yaliyo mabaya, bali iga yaliyo mema.^e

10 *Tnn., "akipiga porojo kutuhusu kwa maneno maovu."

a Mdo 20:29, 30

b Ro 12:10
Flp 2:3
Ebr 13:17

c Zb 101:5
Met 6:16, 19

d Mdo 15:25, 27
Efe 6:21
Flp 2:19
Kol 4:7
Tit 1:5

e Ro 12:9
1Pe 3:11

Safu ya 2

a 1Yo 3:9

b 1Yo 3:6, 10

Mtu anayetenda mema anatokana na Mungu.^a Mtu anayetenda mabaya hajamwona Mungu.^b 12 Demetrio ameshuhudiwa vema nao wote na ile kweli yenyewe. Kwa kweli, sisi pia tunatoa ushahidi kumhusu, nanyi mnajua ushahidi tunaotoa ni wa kweli.

13 Nilikuwa na mambo mengi ya kukuandikia, lakini sitaki kuendelea kukuandikia kwa kalamu na wino. 14 Hata hivyo, ninatumaini kukuona hivi karibuni, nasi tutazungumza uso kwa uso.

Na uwe na amani.

Rafiki wanakutumia salamu zao. Wape rafiki salamu zangu kwa jina.

BARUA YA

YUDA

YALIYOMO

Salamu (1, 2)
Hukumu ya walimu wa uwongo ni hakika (3-16)
Mikaeli abishana na Ibilisi (9)
Unabii wa Enoko (14, 15)

Endeleeni kujitunza katika upendo wa Mungu (17-23)
Kumpa Mungu utukufu (24, 25)

1 Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo, pia ndugu ya Yakobo,^a kwa walioitwa^b ambao wanapendwa na Mungu Baba na kulindwa kwa ajili ya Yesu Kristo:^c

2 Na mzidi kuwa na rehe-ma, amani, na upendo.

3 Wapendwa, ingawa nilikusudia kuwaandikia kuhusu wokovu tulio nao kwa pamo-

a Mt 13:55
Mk 6:3
Gal 2:9
Yak 1:1

b Ebr 3:1
c Yoh 17:15
1Pe 1:5

Safu ya 2

a Ebr 2:3

b Efe 6:11
1Ti 1:18, 19
1Ti 6:12

ja,^a niliona ni lazima niwaandikie ili kuwahimiza mfanye pigano kali kwa ajili ya imani^b ambayo watakatifu walipewa mara moja kwa wakati wote. 4 Kwa maana watu fulani wameingia kisiri kati yenu ambao Maandiko yalisema tangu zamani kwamba wanastahili hukumu; watu hao hawamwogopi Mungu,

wanazitumia fadhili zisizostahiliwa za Mungu wetu kuwa kisingizio cha mwenendo mpo-tovu*^a wakimkana mmiliki*[#] wetu pekee na Bwana wetu, Yesu Kristo.^b

5 Ingawa mnajua vizuri mambo yote haya, nataka kuwakumbusha kwamba ijapokuwa Yehova* aliwaokoa watu kutoka nchi ya Misri,^c baadaye aliwaangamiza wale waliokosa imani.^d **6** Pia malai-ka ambao hawakubaki mahali pao pa kwanza bali walicha makao yao yanayowafaa,^e amewafunga minyororo milele katika giza zito kwa ajili ya hukumu ya ile siku kuu.^f **7** Vivyo hivyo, watu wa Sodom na Gomora na majiji ya karibu walifanya uasherati* wa kupindukia na kufuatilia tamaa za mwili zilizo kinyume cha maumbile;^g wamewekwa mbele yetu kama onyo kwa sababu walihukumiwa adhabu ya moto wa milele.^h

8 Licha ya hayo, watu hawa pia wanajishughulisha na ndoto, wanauchafua mwili, wanadharau mamlaka, na kuwatukana watukufu.ⁱ **9** Lakini Mikaeli,^j yule malaika mkuu^k alipopingana na Ibilisi na kubishana naye kuhusu mwili wa Musa,^l hakuthubutu kumhukumu kwa kumtukana,^m bali alimwambia: "Yehova* na akukeme."ⁿ **10** Lakini watu hawa wanayatukana mambo yote ambayo kwa kweli hawayafahamu.^o Na kuhusu mambo yote wanayoyafahamu

4 *Au "ufidhuli; matendo ya kuchukiza yanayofanywa bila aibu." Kigiriki *a-sel'gei-a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. [#]Au "mkuu." **5, 9, 14** *Angalia Nyongeza A5. **7** *Angalia Kamusi, uku. 2012.

a Gal 5:19
b Mdo 20:29, 30
2Pe 2:1
c Kut 12:41
d Hes 14:35
1Ko 10:1, 5
Ebr 3:16, 19
e Mwa 6:1-4
1Pe 3:19, 20
f Lu 8:30, 31
2Pe 2:4
Ufu 20:1, 2
g Mwa 19:4, 5
Law 18:22
h Mwa 19:24
2Pe 2:6
i Kut 22:28
2Pe 2:10
3Yo 9, 10
j Da 10:21
Da 12:1
k 1Th 4:16
l Kum 34:5, 6
m 2Pe 2:11
n Zek 3:2
o Yud 19

Safu ya 2

a 2Pe 2:12
b Mwa 4:5, 8
1Yo 3:12
c Hes 22:32
2Pe 2:15, 16
Ufu 2:14
d 1Ti 1:20
e Hes 16:3, 32
f 2Pe 2:13
g Eze 34:8
h 2Pe 2:17
i Isa 57:20
j Ebr 6:4-6
Ufu 21:8
k Mwa 5:21, 22
l Kum 33:2
Da 7:10
Zek 14:5
m 2Th 1:6
n Mt 12:36
o 1Ko 10:10
Flp 2:14
p 2Pe 2:18
q Yak 2:9

kiasili kama wanyama wasio na akili,^a wanaendelea kujipotosha wenyewe.

11 Ole wao, kwa sababu wamefuata mwenendo wa Kaini,^b wamejiingiza katika kosa la Balaamu^c ili kupata faida, nao wameangamia katika maneno ya uasi^d ya Kora!^e

12 Hao ndio miamba iliyo chini ya maji katika karamu zenu za kuonyesha upendo^f wanapokula nanyi, wachungaji wanaojilisha bila woga;^g mawingu yasiyo na maji yanayopeperushwa na upepo;^h miti isiyozaa matunda katika majira yake, ambayo imekufa mara mbili* na kung'olewa; **13** mawimbi ya bahari iliyochafuka yenye mapovu ya aibu yao;ⁱ nyota zisizofuata njia hususa, ambazo zitatupwa katika giza zito la milele.^j

14 Enoko,^k wa kizazi cha saba kutoka kwa Adamu, alitabiri pia kuwahusu aliposema: "Tazama! Yehova* alikuja pamoja na maelfu[#] ya watakatifu wake!^l **15** ili kuwahukumu wote,^m na kuwaonyesha wale wasiomwogopa Mungu kwamba wana hatia kwa matendo yao yote ya kutomwogopa Mungu waliyotenda bila kumwogopa Mungu, na kwa maneno yote yenye kushtua ambayo watenda dhambi wasiomwogopa Mungu walisema kumhusu."ⁿ

16 Watu hawa ni wanung'unikaji,^o walalamikaji kuhusu fungu lao maishani, wakifuata tamaa zao wenyewe^p na kujigamba huku wakiwasifusifu wengine* ili wapate faida.^q

12 *Au "imekufa kabisa." **14** *Au "makumi ya maelfu." **16** *Au "kuwastaajabia watu."

17 Lakini ninyi wapendwa, kumbukeni maneno yaliyosemwa zamani* na mitume wa Bwana wetu Yesu Kristo, 18 jinsi walivyokuwa wakiwaambia: “Wakati wa mwisho kutakuwa na wadhihaki, watakaofuata tamaa zao zisizompendeza Mungu.”^a 19 Hao ndio wanaosababisha migawanyiko,^b watu wanaotenda kama wanyama,* wasio na hali ya kiroho.[#] 20 Lakini ninyi wapendwa, jijengeni juu ya imani yenu takatifu zaidi, na kusali mkiwa na roho takatifu,^c 21 ili mwendelee kujitunza katika upendo wa Mungu,^d mkingojea Bwana wetu Yesu Kristo awaonyeshe rehema ili hatimaye mpate uzima wa milele.^e 22 Pia, endele-

17 *Au “yaliyotabiriwa.” 19 *Au “watu wa kimwili.” #Tnn., “roho.”

a Mdo 20:29, 30
1Ti 4:1
2Pe 2:1
2Pe 3:2, 3

b Ro 16:17
3Yo 9, 10

c Ro 8:26
Efe 6:18

d Yoh 15:10
Ro 8:38, 39

e Tit 3:7
1Yo 1:2
1Yo 2:25

Safu ya 2

a Mt 5:7
Mt 9:13
Yak 2:13

b Yak 1:6

c Gal 6:1
Yak 5:19, 20

d Gal 5:19-21

e Ro 8:33
Efe 1:4
Kol 1:22

ni kuwaonyesha rehema^a wale walio na shaka;^b 23 waokoeni^c kwa kuwanyakua kutoka katika moto. Lakini endeleeni kuwaonyesha wengine rehema, mkifanya hivyo kwa woga, huku mkichukia hata vazi ambalo limetiwa doa kupitia mwili.^d

24 Kwake yeye anayeweza kuwalinda ili msijikwae na kuwasaidia msimame bila dosari^e mbele za utukufu wake* mkiwa na shangwe kubwa, 25 kwa Mungu pekee aliye Mwokozi wetu kupitia Yesu Kristo Bwana wetu, kuwe na utukufu, ukuu, nguvu, na mamlaka kwa umilele wote uliopita na sasa na mpaaka umilele wote. Amina.

24 *Au “katika kuwapo kwake kwenye utukufu.”

UFUNUO

KWA YOHANA

YALIYOMO

- Ufunuo kutoka kwa Mungu, kupitia Yesu (1-3)
Salamu kwa yale makutaniko saba (4-8)
“Mimi ndiye Alfa na Omega” (8)
Yohana katika siku ya Bwana kwa mwongozo wa roho (9-11)
Maono ya Yesu aliyetukuzwa (12-20)
- Ujumbe kwa kutaniko la Efeso (1-7), la Smirna (8-11), la Pergamamu (12-17), la Thiatira (18-29)
- Ujumbe kwa kutaniko la Sardisi (1-6), la Filadelfia (7-13), la Laodikia (14-22)
- Aona maono ya Yehova mbinguni (1-11)
Yehova akiwa ameketi kwenye kiti chake cha ufalme (2)

- Wazee 24 kwenye viti vya ufalme (4)
Viumbe hai wanne (6)
- Kitabu cha kukunjwa chenye mihuri saba (1-5)
Mwanakondoo achukua kitabu cha kukunjwa (6-8)
Mwanakondoo anastahili kufungua mihuri (9-14)
- Mwanakondoo afungua mihuri ya kwanza sita (1-17)
Mshindi akiwa kwenye farasi mweupe (1, 2)
Aliyepanda farasi wa rangi ya moto aondoa amani (3, 4)
Aliyepanda farasi mweusi aleta njaa (5, 6)

- Aliyepanda farasi wa kijivu anaitwa Kifo (7, 8)
Walioiua, chini ya madhabahu (9-11)
Tetemeko kubwa la ardhi (12-17)
- 7 Malaika wanne wanaozuia pepo za maangamizi (1-3)
Wale 144,000 watiwa muhuri (4-8)
Umati mkubwa ukiwa umevaa kanzu nyeupe (9-17)
- 8 Muhuri wa saba wafunguliwa (1-6)
Tarumbeta nne za kwanza zapigwa (7-12)
Ole tatu zatangazwa (13)
- 9 Tarumbeta ya tano (1-11)
Ole wa kwanza umepita, mbili zaidi zinakuja (12)
Tarumbeta ya sita (13-21)
- 10 Malaika mwenye nguvu akiwa na kitabu kidogo cha kukunjwa (1-7)
"Hakuna kukawia tena" (6)
Siri takatifu itakamilika (7)
Yohana ala kile kitabu kidogo cha kukunjwa (8-11)
- 11 Mashahidi wawili (1-13)
Watabiri kwa siku 1,260 wakiwa wamevaa nguo za magunia (3)
Wauawa na kuachwa bila kuzikwa (7-10)
Warudishwa kwenye uhai baada ya siku tatu na nusu (11, 12)
Ole wa pili umepita, wa tatu unakuja (14)
Tarumbeta ya saba (15-19)
Ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake (15)
Wale wanaoiharibu dunia wataharibiwa (18)
- 12 Mwanamke, mtoto wa kiume, na joka (1-6)
Mikaeli apigana na yule joka (7-12)
Joka atupwa duniani (9)
Ibilisi anajua kwamba ana kipindi kifupi (12)
Joka amtesa mwanamke (13-17)
- 13 Mnyama-mwitu mwenye vichwa saba atoka baharini (1-10)
Mnyama-mwitu mwenye pembe mbili atoka duniani (11-13)
Sanamu ya mnyama-mwitu mwenye vichwa saba (14, 15)
Alama na namba ya mnyama-mwitu (16-18)
- 14 Mwanakondoo na wale 144,000 (1-5)
Ujumbe kutoka kwa malaika watatu (6-12)
Malaika katikati ya mbingu akiwa na habari njema (6, 7)
Wenye furaha ni wale wanaokufa katika muungano na Kristo (13)
Dunia yavunwa mara mbili (14-20)
- 15 Malaika saba wakiwa na mapigo saba (1-8)
Wimbo wa Musa na wa Mwanakondoo (3, 4)
- 16 Mabakuli saba ya hasira ya Mungu (1-21)
Yamwagwa duniani (2), baharini (3), kwenye mito na chemchemi (4-7), kwenye jua (8, 9), kwenye kiti cha ufalme cha mnyama-mwitu (10, 11), kwenye Mto Efrati (12-16), na hewani (17-21)
Vita vya Mungu, Har-magedoni (14, 16)
- 17 "Babiloni Mkuu" ahukumiwa (1-18)
Kahaba mkubwa aketi juu ya mnyama-mwitu mwenye rangi nyekundu (1-3)
Mnyama-mwitu 'aliyekuwako, lakini hayuko, na bado yuko karibu kupanda kutoka katika shimo refu lisilo na mwisho' (8)
Pembe kumi kupigana na Mwanakondoo (12-14)
Pembe kumi kumchukia kahaba (16, 17)
- 18 "Babiloni Mkuu" aanguka (1-8)
"Tokeni kwake, watu wangu" (4)
Kuombolezea anguko la Babiloni (9-19)
Kushangilia mbinguni kwa sababu ya anguko la Babiloni (20)
Babiloni kutupwa baharini kama jiwe (21-24)
- 19 Msifuni Yah kwa sababu ya hukumu zake (1-10)
Ndoa ya Mwanakondoo (7-9)
Aliyepanda farasi mweupe (11-16)
Mlo mkubwa wa jioni wa Mungu (17, 18)
Mnyama-mwitu ashindwa (19-21)
- 20 Shetani afungwa kwa miaka 1,000 (1-3)
Wale watakaotawala pamoja na Kristo kwa miaka 1,000 (4-6)
Shetani afunguliwa, kisha aangamizwa (7-10)
Wafu wahukumiwa mbele ya kiti cheupe cha ufalme (11-15)

21 Mbingu mpya na dunia mpya (1-8)
Hakuna kifo tena (4)
Mambo yote yafanywa kuwa
mapya (5)
Yerusalemu jipya lafananuliwa (9-27)

22 Mto wa maji ya uzima (1-5)
Umalizio (6-21)
'Njoo! Uchukue maji ya uzima
bure' (17)
"Njoo, Bwana Yesu" (20)

1 Ufunuo* kupitia Yesu Kristo, ambao Mungu alimpa^a ili kuwaonyesha watumwa wake^b mambo yanayopaswa kutukia hivi karibuni. Naye alimtuma malaika wake na kupitia yeye akautoa kwa ishara kwa mtumwa wake Yohana,^c **2** aliyetoa ushahidi kuhusu neno ambalo Mungu alisema na kuhusu ushahidi ambao Yesu Kristo alitoa, ndiyo, kuhusu mambo yote aliyoyaona. **3** Mwenye furaha ni yule anayesoma kwa sauti na wale wanaosikia maneno ya unabii huu, na wanaoshika mambo yaliyoandikwa humo,^d kwa kuwa wakati uliowekwa uko karibu.

4 Yohana, kwa makutaniko saba^e yaliyo katika mkoa wa Asia:

Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani kutoka kwa "Yule aliyeko na aliyekuwako na anayekuja,"^f na kutoka kwa zile roho saba^g zilizo mbele ya kiti chake cha ufalme, **5** na kutoka kwa Yesu Kristo, "Shahidi Mwaminifu,"^h "mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu,"ⁱ na "Mtawala wa wafalme wa dunia."^j

Yeye anayetupenda^k na aliyetuweka huru kutoka katika dhambi zetu kupitia damu yake mwenyewe!— **6** naye alitufanya tuwe ufalme,^m ma-

1:1 *Au "Kufichua siri."

SURA YA 1

a Da 2:28
b Amo 3:7
Ufu 7:3, 4
c Mt 10:2
Mk 1:19
Yoh 21:20
d Zb 1:2
Lu 11:28
Yoh 13:17
Yak 1:22
e Ufu 1:11
f Ufu 1:8
Ufu 4:8
Ufu 11:17
g Ufu 4:5
h Ufu 3:14
i Kol 1:18
j Zb 89:27
1Ti 6:15
Ufu 19:16
k Yoh 15:9
l Ebr 9:14
1Pe 1:18, 19
1Yo 1:7
m Kut 19:6
Lu 22:28-30

Safu ya 2

a 1Pe 2:5
Ufu 5:9, 10
Ufu 20:6
b Mt 26:64
Mk 13:26
c Mt 24:30
d Isa 48:12
Ufu 21:6
Ufu 22:13
e Kut 6:3
f Mt 24:9
g Lu 12:32
h Mt 10:22
2Ti 2:12
i Ro 8:17
j Efe 1:1
Ufu 2:1
k Ufu 2:8
l Ufu 2:12
m Ufu 2:18
n Ufu 3:1
o Ufu 3:7
p Ufu 3:14

kuhani^a kwa Mungu na Baba yake—ndiyo, na awe na utukufu na nguvu milele. Amina.

7 Tazama! Anakuja na mawingu,^b na kila jicho litamwona, na wale waliomchoma,* na makabila yote ya dunia yatajipigapiga kwa huzuni kwa sababu yake.^c Ndiyo, Amina.

8 "Mimi ndiye Alfa na Omega,"^{*d} asema Yehova[#] Mungu, "Yule aliyeko na aliyekuwako na anayekuja, Mweza-Yote."^e

9 Mimi Yohana, ndugu yenu na mshiriki pamoja nanyi katika dhiki^f na ufalme^g na uvumilivu^h katika ushirika na Yesu,ⁱ nilikuwa katika kisiwa kinachoitwa Patmo kwa sababu ya kuzungumza kumhusu Mungu na kutoa ushahidi kumhusu Yesu. **10** Kwa mwongozo wa roho nilikuja kuwa katika siku ya Bwana, nami nikasikia nyuma yangu sauti yenye nguvu kama ya tarumbeta, **11** iki-sema: "Yale unayoona, yandike katika kitabu cha kunkunjwa kisha uyatume kwa yule makutaniko saba: katika Efeso,^j katika Smirna,^k katika Pergamamu,^l katika Thiatira,^m katika Sardi,ⁿ katika Filadelfia,^o na katika Laodikia."^p

12 Nikageuka ili nimwone yule aliyekuwako akizungumza

1:7 *Au "waliomdunga." 1:8 *Au "herufi A na Z." Alfa ni herufi ya kwanza na Omega ni herufi ya mwisho katika alfabeti ya Kigiriki. #Angalia Nyongeza A5.

nami, nilipogeuka, nikaona vinara saba vya taa vya dhahabu,^a **13** na katikati ya vinara hivyo vya taa palikuwa na mtu kama mwana wa binadamu,^b aliyevaa vazi lililofika chini miguuni na kifua-ni alikuwa amevaa mshipi wa dhahabu. **14** Zaidi ya hayo, kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji, na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto,^c **15** na miguu yake ilikuwa kama shaba safi^d inapowaka katika tanuru, na sauti yake ilikuwa kama sauti ya maji mengi. **16** Na kwenye mkono wake wa kuume kulikuwa na nyota saba,^e na kutoka katika kinywa chake upanga mkali, mrefu, wenyewe makali pande mbili^f ulikuwa umechomoza, na sura yake ilikuwa* kama jua lina-pong'aa kabisa.^g **17** Nilipomwona, nikaanguka miguuni pake kana kwamba nimekufa.

Naye akaweka mkono wake wa kuume juu yangu na kusema: "Usiogoep. Mimi ndiye wa Kwanza^h na wa Mwisho,ⁱ **18** na aliye hai,^j nami niliku-fa,^k lakini tazama! ninaishi milele na milele,^l nami nina funguo za kifo na za Kaburi.*^m **19** Kwa hiyo andika mambo uliyooona, na mambo yaliyopo, na mambo yatakayotukia baada ya haya. **20** Kuhusu siri takatifu ya zile nyota saba ulizooona kwenye mkono wangu wa kuume, na ya vile vinara saba vya taa vya dhahabu: Zile nyota saba zinamaanisha wale malaika wa yale makutaniko saba, na vile vi-

1:16 *Au "uso wake ulikuwa." 1:18 *Au "Hadesi." Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 1

- a Ufu 1:20
b Da 7:13
c Ufu 19:12
d Ufu 2:18
e Ufu 1:20
f Isa 49:2
g Mt 17:1, 2
h Mdo 26:23
Kol 1:18
Ufu 1:5
i Ufu 2:8
j 1Ko 15:45
k 1Pe 3:18
l Ro 6:9
ITI 6:16
m Mt 16:18
Yoh 6:54
Yoh 11:25

Safu ya 2

- a Mt 5:16
Flp 2:15

SURA YA 2

- b Ufu 1:20
c Mdo 19:1
Efe 1:1
d Ufu 1:12, 13
e Mdo 20:29, 30
2Ko 11:13
1Yo 4:1
f 1Pe 4:14
g Gal 6:9
h Ufu 3:19
i Ufu 1:20
j Ufu 2:16
k 1Ko 11:19
Ufu 2:15
l Mt 11:15
Ufu 2:17, 29
m 1Yo 5:4
n Ro 2:6, 7
Ufu 2:10
o Ufu 1:13, 17
p Ro 14:9

nara saba vya taa vinamaanisha yale makutaniko saba.^a

2 "Kwa malaika^b wa kutaniko lililo huko Efeso^c andika: Haya ndiyo mambo anayosema yule anayeshika zile nyota saba kwenye mkono wake wa kuume, na kutembea kati ya vile vinara saba vya taa vya dhahabu:^d **2** 'Ninajajua matendo yako, na kazi yako ya jasho na uvumilivu, na kwamba huwavamilii watu wabaya, nawe unawajaribu wale wanaosema kwamba wao ni mitume,^e lakini wao sio, nawe uliwagundua kuwa waongo. **3** Wewe pia unaoonyesha uvumilivu, na umestahimili kwa ajili ya jina langu^f nawe hujachoka.^g **4** Hata hivyo, nina jambo hili dhidi yako, kwamba umeacha upendo uliokuwa nao mwanzoni.

5 "Kwa hiyo kumbuka pale ulipokuwa kabla ya kuanguka, nawe utubu^h na kufanya matendo uliyofanya mwanzoni. Usipofanya hivyo, nitakuja kwako, nami nitakiiondoa kinara chako cha taaⁱ kutoka mahali pake, usipotubu.^j **6** Hata hivyo, ninakusifu kwa jambo hili: kwamba unachukia matendo ya madhehebu ya Nikolao,^k ambayo mimi pia ninayachukia. **7** Yule aliyenye na sikio na asikie yale ambayo roho inayaambia makutaniko:^l Yule atakayeshinda^m nitampa ruhusa ya kula matunda ya ule mti wa uzima,ⁿ ulio katika paradiso ya Mungu.^o

8 "Na kwa malaika wa kutaniko lililo huko Smirna andika: Haya ndiyo mambo anayosema, 'wa Kwanza na wa Mwisho,^o aliyekufa na akawa hai tena:^p **9** 'Ninajua dhiki na umaskini wako—lakini

wewe ni tajiri^a—na kufuru la wale wanaojiita Wayahudi na kwa kweli sio, bali wao ni sinagoga la Shetani.^b **10** Usiogope mateso yatakayokupata hivi karibuni.^c Tazama! Ibilisi ataendelea kuwatupa gerezeni baadhi yenu ili mjaribiwe kwa ukamili, nanyi mtapata dhiki kwa siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufikia kifo, nami nitakupa taji la uzima.^d **11** Yule aliye na sikio na asikie^e yale ambayo roho inayaaambia makutaniko: Yule atakayeshinda,^f kifo cha pili hakitamduru hata kidogo.^g

12 “Kwa malaika wa kutaniko lililo huko Pergamamu andika: Haya ndiyo mambo anayosema yule aliye na ule upanga mkali, mrefu na wenyewe makali pande mbili:^h **13** ‘Ninajua mahali anapokaa, yaani, mahali kilipo kiti cha ufalme cha Shetani; lakini bado unaendelea kulishika imara jina langu,ⁱ nawe hukukana imani yako kwangu^j hata katika siku za Antipa, shahidi wangu mwaminifu^k aliyeuawa^l kando yenu, mahali anapokaa Shetani.

14 “Hata hivyo, nina mambo machache dhidi yako, kwamba unao hapo wale wanaofuata fundisho la Balaamu,^m aliyemfundisha Balakiⁿ kuweka kikwazo mbele ya wana wa Israeli, ili wale vitu vilivyotolewa dhahihu kwa sanamu na kufanya uasherati.^o **15** Vivyo hivyo, pia una wale wanaofuata fundisho la madhehebu ya Nikolao.^p **16** Basi tubu. Usipofanya hivyo, ninakuja kwako upesi, nami nitapigana nao

2:14, 20 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 2

a 2Ko 6:4, 10
1Ti 6:18, 19
Yak 2:5

b Ufu 3:9

c Mt 10:28

d Ro 2:6, 7
2Ti 4:7, 8
Yak 1:12
Ufu 20:4

e Ufu 13:9

f 1Yo 5:5

g Ufu 20:6
Ufu 20:14
Ufu 21:8

h Ufu 1:13, 16
Ufu 19:15

i Mk 13:9
Ufu 2:3

j Lu 12:8
1Yo 2:23

k Mdo 1:8

l Mt 24:9

m Hes 31:16
2Pe 2:15
Yud 11

n Hes 22:4

o Hes 25:1, 2
Mdo 15:28, 29
Efe 5:5

p 2Pe 2:1
Ufu 2:6

Safu ya 2

a Ufu 1:13, 16

b Ufu 2:7

c 1Yo 5:5
Ufu 3:12

d Kut 16:15, 31
Zb 78:24
Ebr 9:4

e Mdo 16:14

f Ufu 19:12

g Ufu 1:13-15

h 1Fa 16:31
2Fa 9:22

i 1Ko 5:11
Gal 5:19
Efe 5:5

kwa ule upanga mrefu wa kinywa changu.^a

17 “Yule aliye na sikio na asikie yale ambayo roho inayaaambia makutaniko:^b Yule atakayeshinda^c nitampa baadhi ya mana iliyofichwa,^d nami nitampa jiwe dogo jeupe, na kwenye jiwe hilo, jina jipya limeandikwa ambalo hakuna yeyote anayelijua ila yule anayelipokea.’

18 “Kwa malaika wa kutaniko lililo huko Thiatira^e andika: Haya ndiyo mambo anayosema Mwana wa Mungu, ambaye macho yake ni kama mwali wa moto^f na ambaye miguu yake ni kama shaba safi:^g **19** ‘Ninayajua matendo yako, na upendo wako na imani na huduma na uvumilivu wako, na kwamba matendo yako ya hivi karibuni yanazidi yale uliyofanya mwanzoni.

20 “Hata hivyo, nina jambo hili dhidi yako, kwamba unamvumilia yule mwanamke Yezabeli,^h anayejiita nabii, naye anafundisha na kuwapotosha watumwa wangu wafanye uasheratiⁱ na kula vitu vilivyotolewa dhahihu kwa sanamu.

21 Nami nilipma muda wa kutubu, lakini hataki kutubu uasherati^{*} wake. **22** Tazama! niko karibu kumtupa katika kitanda cha ugonjwa, na kuwatupa katika dhiki kuu wale wanaofanya uzinzi pamoja naye, ikiwa hawatatubu matendo yake. **23** Nami nitawaua watoto wake kwa ugonjwa hatari, hivi kwamba makutaniko yote yatajua kwamba mimi ndiye ninayechunguza mwazo ya ndani kabisa^{*} na mioyo, nami

2:21 *Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 2:23 *Au “hisia za ndani kabisa.” Tnn., “figo.”

nitampa kila mmoja wenu kulingana na matendo yake.^a

24 “Hata hivyo, ninawambia wale wengine kati yenu walio huko Thiatira, wote wasiofuata fundisho hili, wale ambao hawakujua yale yanayoitwa “mambo mazito ya Shetani”:^b Mimi siwaongezei mzigo mwingine wowote. **25** Hata hivyo, shikeni imara lile mlilo nalo mpaka nitakapokuja.^c

26 Na yule atakayeshinda na kushika matendo yangu mpaka mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa,^d **27** kama vile nilivyopokea kutoka kwa Baba yangu, naye atawachunga watu kwa fimbo ya chuma^e hivi kwamba watawunjwa vipandevipande kama vyombo vya udongo. **28** Nami nitampa nyota ya asubuhi.^f **29** Yule aliye na sikio na asikie yale ambayo roho inayaambia makutaniko.’

3 “Kwa malaika wa kutaniko lililo huko Sardi andika: Haya ndiyo mambo anayosema yule aliye na zile roho saba za Mungu^g na zile nyota saba:^h ‘Ninayajua mateendo yako, kwamba una jina* kuwa uko hai, lakini umekufa.ⁱ **2** Uwe macho,^j na uyatie nguvu mambo yanayobaki yaliyokuwa tayari kufa, kwa maana mimi sikuona kazi zako zikiwa zimefanywa kikamili* mbele za Mungu wangu. **3** Kwa hiyo, endelea kuzingatia* jinsi ulivyopokea na jinsi ulivyosikia, na uendeleo kulishika, na utubu.^k Hakika usipoamka, nitakuja kama mwizi,^l nawe hutajua kamwe saa nitakayokuja juu yako.^m

3:1 *Au “unajulikana.” 3:2 *Au “zimekamilika.” 3:3 *Au “kukumbuka.”

SURA YA 2

a Ufu 22:12

b Yoh 8:44

c Ufu 3:11

d Zb 2:8, 9
Mt 19:28
Lu 22:28-30
Ufu 3:21
Ufu 20:4e Ufu 12:5
Ufu 19:15

f Ufu 22:16

SURA YA 3

g Ufu 1:4
Ufu 4:5

h Ufu 1:13, 16

i Yak 2:26

j Lu 21:34
Efe 5:15
1Th 5:6

k 2Ko 7:11

l Ufu 16:15

m Mt 24:42
Lu 12:37, 39

Safu ya 2

a Yak 1:27

b Ufu 6:11

c 1Yo 5:4

d Ufu 4:4
Ufu 19:8

e Flp 4:3

f Lu 12:8

g Yoh 6:69
Ebr 7:26h Ufu 3:14
Ufu 19:11i Isa 22:22
Lu 1:32j 1Ko 16:9
2Ko 2:12k Ro 2:28
Ufu 2:9l Lu 8:15
Lu 21:19
2Ti 2:12
Ebr 10:36
Ebr 12:3

m 2Th 3:3

4 “Hata hivyo, una watu wachache* katika Sardi ambao hawakuyatia unajisi mavazi yao,^a nao watatembea pamoja nami wakiwa na mavazi meupe,^b kwa sababu wanastahili.

5 Kwa hiyo, yule atakayeshinda^c atavikwa mavazi meupe,^d na kwa vyovyote sitalifuta* jina lake kutoka katika kitabu cha uzima,^e bali nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele ya malaika zake.^f

6 Yule aliye na sikio na asikie yale ambayo roho inayaambia makutaniko.’

7 “Kwa malaika wa kutaniko lililo huko Filadelfia andika: Haya ndiyo mambo anayosema yule aliye mtakatifu,^g aliye wa kweli,^h aliye na ufunguo wa Daudi,ⁱ anayefungua hivi kwamba hakuna yeyote atakayefunga na anayefunga hivi kwamba hakuna yeyote anayefungua: **8** ‘Ninayajua matendo yako—tazama! nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa,^j usioweza kufungua na yeyote. Nami ninajua kwamba una nguvu kidogo, nawe ulilishika neno langu na hukulikana jina langu.

9 Tazama! Nitawafanya wale wa sinagogi la Shetani wanaosema ni Wayahudi ingawa sio,^k lakini wanasema uwongo—tazama! nitawafanya waje wainame* mbele ya miguu yako na kuwafanya wajue kwamba nimekupenda wewe. **10** Kwa sababu ulilishika neno kuhusu uvumilivu wangu,^l mimi pia nitakulinda kutokana na ile saa ya jaribu^m itakayokuja juu ya dunia nzima ina-

3:4 *Tnn., “majina machache.” 3:5 *Au “sitaliondoa.” 3:9 *Au “wasujudu.” 3:10 *Au labda, “ulifuata mfano wangu wa uvumilivu.”

yokaliwa, ili kuwajaribu wale wanaokaa duniani. **11** Nina-kuja upesi.^a Endelea kushika imara kile ulicho nacho, ili yeyote asilichukue taji lako.^b

12 “Yule atakayeshinda –nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, naye hataondoka humo kamwe, nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu^c na jina la jiji la Mungu wangu, Yerusalemu Jipya^d linaloshuka kutoka mbinguni kwa Mungu wangu, na jina langu jipya.^e **13** Yule aliye na sikio na asikie yale ambayo roho inayambia makutaniko.’

14 “Kwa malaika wa kutaniko lililo huko Laodikia^f andika: Haya ndiyo mambo anayosema Amina,^g shahidi^h mwaminifu na wa kweli,ⁱ mwanzo wa uumbaji wa Mungu.^j **15** ‘Ninayajua matendo yako, kwamba wewe si baridi wala si moto. Laiti ungekuwa bari-di au moto. **16** Basi kwa sababu wewe ni vuguvugu na si moto^k wala si baridi,^l nitakutapika kutoka kinywani mwangu. **17** Kwa sababu unase-ma, “Mimi ni tajiri,^m nimejipatia utajiri na sihitaji kitu chochote,” lakini hujui kwamba wewe ni mwenye taabu na wa kusikitikiwa na maskini na kipofu na uko uchi, **18** ninakushauri ununue kutoka kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili uwe tajiri, na mavazi meupe ili uvae na kwamba aibu ya uchi wako isifunuliwe,ⁿ na dawa ya macho ya kupaka katika macho yako^o ili uweze kuona.^p

19 “Wale wote ninaowapenda, mimi huwakaripia na kuwatia nidhamu.^q Basi uwe mwenye bidii na utubu.^r

SURA YA 3

- a Ufu 2:16
b Yak 1:12
Ufu 2:10
c Ufu 22:3, 4
d Ebr 12:22
Ufu 21:2
e Ufu 14:1
Ufu 19:12
f Kol 4:16
g 2Ko 1:20
h Yoh 18:37
1Ti 6:13
Ufu 1:5
i Yoh 1:14
Ufu 19:11
j Met 8:22
Kol 1:15
k 2Ko 9:2
l Met 25:13
m Ho 12:8
n Ufu 16:15
o Zb 19:8
p 1Ti 6:17-19
q Met 3:12
r Ufu 2:5
Ufu 3:3

Safu ya 2

- a 1Yo 5:4
Ufu 12:11
b Mt 19:28
Lu 22:28-30
Ufu 2:26
c Ebr 10:12

SURA YA 4

- d 1Fa 22:19
Isa 6:1
Eze 1:26, 27
Da 7:9
Mdo 7:55
e Ufu 21:10, 11
f 1Yo 1:5
g Ufu 4:10
Ufu 5:8
Ufu 11:16
Ufu 19:4
h Eze 1:13
i Kut 19:16
j Ufu 1:4
Ufu 5:6

20 Tazama! Nimesimama mlangoni na ninapiga hodi. Mtu yeyote akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango, nitaingia ndani ya nyumba yake na kula mlo wa jioni pamoja naye, naye pamoja nami. **21** Yule atakayeshinda^a nitampa ruhusa ya kuketi pamoja nami kwenye kiti changu cha ufalme,^b kama vile nilivyoshinda na kuketi^c pamoja na Baba yangu kwenye kiti chake cha ufalme. **22** Yule aliye na sikio na asikie yale ambayo roho inayambia makutaniko.”

4 Baada ya hayo nikaona, na tazama! mlango uliofunguliwa mbinguni, na sauti ya kwanza niliyoisikia ikizungumza nami ilikuwa kama ya tarumbeta, ikisema: “Panda uje huku, nami nitakuonyesha mambo ambayo lazima yatendeke.” **2** Baada ya hayo mara moja nikawa katika nguvu za roho, na tazama! kiti cha ufalme kilikuwa mahali pake mbinguni, na kulikuwa na mtu aliyeketi kwenye kile kiti.^d

3 Na Yule aliyeketi alionekana kama jiwe la yaspi^e na jiwe je-kundu lenye thamani, na kuzunguka kile kiti cha ufalme kulikuwa na upinde wa mvua ulioonekana kama zumaridi.^f

4 Kuzunguka kile kiti cha ufalme kulikuwa na viti vya ufalme 24, na kwenye viti hivyo vya ufalme niliona wameketi wazee 24^g waliovaa mavazi meupe, na juu ya vichwa vyao mataji ya dhahabu.

5 Kwenye kile kiti cha ufalme kulitokea radi^h na sauti na ngurumo;ⁱ na kulikuwa na taa saba za moto zikiwaka mbele ya kile kiti cha ufalme, ambazo zinamaanisha zile roho saba za Mungu.^j **6** Mbele ya

kile kiti cha ufalme kulikuwa na kitu kinachofanana na bahari ya kioo,^a kama fuwele.

Katikati ya kile kiti cha ufalme* na kuzunguka kile kiti kulikuwa na viumbe hai wanne^b waliojaa macho mbele na nyuma. **7** Kiumbe hai wa kwanza alikuwa kama simba,^c na kiumbe hai wa pili alikuwa kama ng'ombe dume mchanga,^d na kiumbe hai wa tatu^e alikuwa na uso kama wa mwanadamu, na kiumbe hai wa nne^f alikuwa kama tai anayeruka.^g **8** Kuhusu wale viumbe hai wanne, kila mmoja wao alikuwa na mabawa sita; walikuwa na macho kila mahali pande zote na chini yao.^h Na mchana na usiku wanaendelea kusema: "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Yehovaⁱ Mungu, Mweza-Yote, aliyekuwako na aliyeko na anayekuja."^j

9 Kila mara wale viumbe hai wanapompa utukufu na heshima na shukrani Yule anayeketi kwenye kile kiti cha ufalme, Yule anayeishi milele na milele,^k **10** wale wazee 24^l huanzuka chini mbele za Yule anayeketi kwenye kile kiti cha ufalme na kumwabudu Yule anayeishi milele na milele, nao hutupa mataji yao mbele ya kile kiti wakisema: **11** "Unastahili, Ee Yehova* Mungu wetu, kupokea utukufu^m na heshima" na nguvu,^o kwa sababu uliumba vitu vyote,^p na kwa sababu ya mapenzi yako vilitokea navyo vikaumbwa."

5 Nami nikaona katika mkonono wa kuume wa Yule aliyeketi kwenye kile kiti cha ufalme,^q kitabu cha kukunjwa

4:6 *Au "Katikati pamoja na kile kiti cha ufalme." 4:8, 11 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 4

- a Kut 30:18
1Fa 7:23
b Eze 1:5-10
c Met 28:1
Isa 31:4
d Ayu 39:9-11
Ufu 6:3
e Ufu 6:5
f Ufu 6:7
g Ayu 39:27, 29
Eze 1:10
h Eze 10:9, 12
i Isa 6:2, 3
j Ufu 1:4
k Zb 90:2
Da 12:7
l Ufu 5:8
m Mt 5:16
Ufu 14:7
n Ufu 19:10
o Ufu 5:13
Ufu 7:12
Ufu 11:17
Ufu 12:10
p Ufu 10:6

SURA YA 5

- q Ufu 4:2, 3
Safu ya 2
a Mwa 49:9, 10
Ebr 7:14
b Isa 11:1, 10
Ro 15:12
c 2Sa 7:8, 12
Ufu 22:16
d Yoh 16:33
e Isa 53:7
Yoh 1:29
1Pe 1:19
f Yoh 19:30
Ufu 5:12
g Efe 1:22
h Ufu 1:4
i Zb 47:8
Isa 6:1
j Ufu 5:14
Ufu 19:4

mbili,* kilichofungwa kabisa kwa mihuri saba. **2** Nami nikamwona malaika mwenye nguvu akitangaza kwa sauti kubwa: "Ni nani anayestahili kukifungua kile kitabu cha kukunjwa na kuvunja mihuri yake?" **3** Lakini hakuna yeyote mbinguni au duniani au chini ya dunia aliyeweza kukifungua kitabu hicho cha kukunjwa au kutazama ndani yake. **4** Nikalia sana kwa sababu hakupatikana yeyote aliyestahili kukifungua kitabu hicho cha kukunjwa au kutazama ndani yake. **5** Lakini mmoja wa wale wazee akaniaambia: "Acha kulia. Tazama! Simba wa kabila la Yuda,^a mzizi^b wa Daudi,^c ameshinda^d ili akiifungua kitabu hicho cha kukunjwa na mihuri yake saba."

6 Nami nikamwona mwana-kondoo^e aliyeonekana kana kwamba amechinjwa,^f akiwa amesimama katikati ya kile kiti cha ufalme na katikati ya wale viumbe hai wanne na katikati ya wale wazee,^g akiwa na pembe saba na macho saba, na macho hayo yanamaanisha roho saba za Mungu^h ambazo zimetumwa katika dunia nzima. **7** Mara moja akaja na kukichukua kutoka katika mkono wa kuume wa Yule aliyeketi kwenye kile kiti cha ufalme.ⁱ **8** Alipokichukua kile kitabu cha kukunjwa, wale viumbe hai wanne na wale wazee 24^l wakaanguka chini mbele ya Mwanakondoo, na kila mmoja alikuwa na kinubi na mabakuli ya dhahabu yaliyojaa uvumba. (Uvumba huo unamaanisha sala za

5:1 *Tnr., "upande wa ndani na wa nyuma."

watakatifu.)^a **9** Nao wanaimba wimbo mpya,^b wakisema: “Wewe unastahili kukichukua kile kitabu cha kukunjwa na kufungua mihuri yake, kwa sababu ulichinjwa na kwa damu yako ukamnunulia Mungu watu^c kutoka katika kila kabila na lugha na watu na taifa,^d **10** na ukawafanya kuwa ufalme^e na makuhani kwa Mungu wetu,^f nao watatawala dunia wakiwa wafalme.”^g

11 Nami nikaona, na kusikia sauti ya malaika wengi kuzunguka kile kiti cha ufalme na wale viumbe hai na wale wazee, na idadi yao ilikuwa makumi ya maelfu ya makumi ya maelfu na maelfu ya maelfu,^h **12** nao walikuwa wakisema kwa sauti kubwa: “Mwanakondoo aliyechinjwaⁱ anastahili kupokea uwezo na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.”^j

13 Nami nikasikia kila kiumbe kilicho mbinguni na duniani na chini ya dunia^k na baharini, na vitu vyote vilivyondani yake, vikisema: “Yule anayeketi kwenye kile kiti cha ufalme^l na Mwanakondoo^m na wawe na baraka na heshimaⁿ na utukufu na nguvu milele na milele.”^o **14** Wale viumbe hai wanne walikuwa wakisema: “Amina!” na wale wazee wakaanguka chini na kuabudu.

6 Naye Mwanakondoo^p alipofungua mmoja wa ile mihuri saba,^q nikaona, na kumsikia mmoja wa wale viumbe hai wanne^r akisema kwa sauti kama ya ngurumo: “Njoo!” **2** Nami nikaona, na tazama! farasi mweupe,^s na yule aliyeketi juu yake alikuwa na upinde; naye akapewa taji,^t naye

SURA YA 5

- a Zb 141:2
Ufu 8:4
b Zb 33:3
Zb 144:9
Isa 42:10
Ufu 14:3
c Mt 26:27, 28
1Ko 6:20
Ebr 9:12
1Pe 1:18, 19
d Ufu 14:4
e Lu 12:32
Lu 22:28-30
f Kut 19:6
1Pe 2:9
Ufu 1:5, 6
g Mt 19:28
Ufu 20:4, 6
Ufu 22:5
h Da 7:9, 10
i Isa 53:7
Ufu 5:6
j Mt 28:18
k Flp 2:9, 10
l Ufu 4:2, 3
m Yoh 1:29
Ufu 7:17
n Yoh 5:23
1Ti 6:16
o 1Pe 4:11

SURA YA 6

- p Ufu 5:6
q Ufu 5:5
r Ufu 4:7
s Ufu 19:11
t Ufu 14:14

Safu ya 2

- a Zb 45:4
Zb 110:1, 2
Ufu 12:7
Ufu 17:14
b Ufu 4:7
c Mt 24:7
Lu 21:10
d Ufu 5:5
e Ufu 4:7
f Mt 20:2
g Mk 13:8
h Ufu 4:7
i Lu 21:11
j Yer 15:2, 3
Eze 14:21
k Law 4:7
Ufu 8:3
l Law 17:11

akaenda akishinda na kukamilisha ushindi wake.^a

3 Alipofungua muhuri wa pili, nikamsikia kiumbe hai wa pili^b akisema: “Njoo!” **4** Mwingine akatokea, farasi mwe nye rangi ya moto, na yule aliyeketi juu yake akapewa ruhusa ya kuondoa amani duniani ili wauane, naye akapewa upanga mkubwa.^c

5 Alipofungua muhuri wa tatu,^d nikamsikia kiumbe hai wa tatu^e akisema: “Njoo!” Nami nikaona, na tazama! farasi mweusi, na yule aliyeketi juu yake alikuwa na mizani mkononi mwake. **6** Nami nikasikia kitu kama sauti kati kati ya wale viumbe hai wanne ikisema: “Kibaba* cha ngano kwa dinari^{ff} moja na vibaba vitatu vya shayiri kwa dinari moja; na usidhuru divai na mafuta ya zeituni.”^g

7 Alipofungua muhuri wa nne, nikasikia sauti ya kiumbe hai wa nne^h akisema: “Njoo!” **8** Nami nikaona, na tazama! farasi wa rangi ya kijivu, na yule aliyeketi juu yake alikuwa na jina Kifo. Na Kaburi* lilikuwa likimfuata kwa ukaribu. Nao wakapewa mamlaka juu ya sehemu ya nne ya dunia, ili kuua kwa upanga mrefu na kwa upungufu wa chakulaⁱ na kwa ugonjwa hatari na kwa wanyama wa mwituni wa dunia.^j

9 Alipofungua muhuri wa tano, nikaona chini ya madhabahu^k nafsi*^l za wale

6:6 *Angalia Nyongeza B14. #Sarafu ya fedha ya Kiroma iliyolingana na mshahara wa siku moja. Angalia Nyongeza B14. **6:8** *Au “Hadesi.” Angalia Kamusi, uku. 2012. **6:9** *Inaonekana ni uhai unaowakilishwa na damu yao iliyomwagwa kwenye madhabahu. Angalia Kamusi, uku. 2012.

waliouawa kwa sababu ya neno la Mungu na kwa sababu ya ushahidi waliokuwa wame-toa.^a **10** Wakasema kwa sauti kubwa: “Bwana Mwenye Enzi Kuu, mtakatifu na wa kweli,^b utajizua mpaka lini kuhukumu na kulipiza kisasi cha damu yetu juu ya wale wanaokaa duniani?”^c **11** Na kila mmoja wao akapewa kanzu nyeupe,^d nao wakaambiwa waendelee kupumzika kwa muda mfupi, mpaka idadi itimie ya watumwa wenzao na ndugu zao waliokuwa karibu kuuuawa kama vile wao wali-vyuuawa.^e

12 Nami nikaona alipofungua muhuri wa sita, na tete-meko kubwa la ardhi likatokea; na jua likawa jeusi kama gunia la manyoya,^{*} na mwezi mzima ukawa kama damu,^f **13** na nyota za mbinguni zikaanguka duniani kama mtini unaotikiswa na upepo mkali unavyoangusha tini zake mbi-chi. **14** Na mbingu ikaondoka kama kitabu cha kukunjwa kinachokunjwa,^g na kila mlima na kila kisiwa vikaondolewa mahali pake.^h **15** Na wafalme wa dunia, maofisa wa cheo cha juu, viongozi wa kijeshi, matajiri, wenye nguvu, kila mtumwa, na kila mtu aliyehuru wakajificha katika mapango na katika miamba ya milima.ⁱ **16** Nao wanaendelea kuiambia milima na miamba: “Tuangukieni,^j mtufiche kuto-ka kwenye uso wa Yule anayeketi kwenye kile kiti cha ufal-me^k na kutoka kwenye ghadhabu ya Mwanakondoo,^l **17** kwa sababu siku kuu ya ghadhabu yao imekuja,^m

6:12 *Huenda lililotengenezwa kwa manyoya ya mbuzi.

SURA YA 6

a Mt 24:9, 14
Yoh 18:37
Ufu 17:6
Ufu 20:4

b 1Yo 5:20

c Kum 32:43
Lu 18:7
Ufu 19:1, 2

d Ufu 3:5

e Mt 24:9
Mdo 9:1
2Ko 1:8

f Yoe 2:31
Mt 24:29

g Isa 34:4

h Ufu 16:20

i Isa 2:10, 19

j Ho 10:8
Lu 23:30

k Ufu 4:2, 3

l Ufu 5:6

m Sef 1:14, 18
Ro 2:5

Safu ya 2

a Yoe 2:11

SURA YA 7

b 2Ko 1:22
Efe 1:13
Efe 4:30

c Ufu 9:4

d Ufu 14:1, 3

e Ro 2:29
Ro 9:6
Gal 6:16
Ufu 21:12

f Mwa 41:51

na ni nani anayeweza kusi-mama?”^a

7 Baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesima-ma juu ya pembe nne za dunia, wakizishika kwa nguvu zile pepo nne za dunia ili upepo wowote usivume juu ya dunia au juu ya bahari au juu ya mti wowote. **2** Nami nikamwona malaika mwingine akipanda kutoka mashariki,^{*} akiwa na muhuri wa Mungu aliyehai; naye akawaambia kwa sauti kubwa wale malai-ka wanne waliopewa ruhusa ya kuidhuru dunia na bahari, **3** akisema: “Msiidhuru dunia au bahari au miti, hadi tuta-kapwatia muhuri^b watumwa wa Mungu wetu katika mapaji ya nyuso zao.”^c

4 Nami nikaisikia idadi ya wale waliotiwa muhuri, 144,-000,^d waliotiwa muhuri kutoka kila kabila la wana wa Israeli:^e

5 Kutoka kabila la Yuda 12,000 waliotiwa muhuri; kutoka kabila la Rubeni 12,000;

kutoka kabila la Gadi 12,000; kutoka kabila la Asheri 12,000;

kutoka kabila la Naftali 12,000;

kutoka kabila la Manase^f 12,000;

7 kutoka kabila la Simeoni 12,000;

kutoka kabila la Lawi 12,000;

kutoka kabila la Isakari 12,000;

8 kutoka kabila la Zabuloni 12,000;

kutoka kabila la Yosefu 12,000;

7:2 *Au “mawio ya jua.”

kutoka kabila la Benjamini 12,000 walioitiwa muhuri.

9 Baada ya hapo nikaona, na tazama! umati mkubwa, ambao hakuna mtu aliyeweza kuuhesabu, kutoka mataifa yote na makabila na jamii na lugha,^a wakiwa wamesimama mbele ya kiti cha ufalme na mbele ya Mwanakondoo, wakiwa wamevaa kanzu nyeupe;^b na walikuwa na matawi ya mitende mikononi mwao.^c

10 Nao wanaendelea kusema kwa sauti kubwa: "Wokovu unatoka kwa Mungu wetu, anayeketi kwenye kiti cha ufalme,^d na kwa Mwanakondoo."^e

11 Malaika wote walikuwa wamesimama kukizunguka kile kiti cha ufalme na wale wazee^f na wale viumbe hai wanne, nao wakaanguka kifudufudi mbele ya kile kiti cha ufalme na kumwabudu Mungu, **12** wakisema: "Amina! Sifa na utukufu na hekima na shukrani na heshima na uwezo na nguvu ziwe kwa Mungu wetu milele na milele.^g Amina."

13 Ndipo mmoja wa wale wazee akaniuliza: "Hawa waliovaa kanzu nyeupe,^h ni nani nao walitoka wapi?" **14** Basi nikamwambia mara moja: "Bwana wangu, wewe ndiye unayejua." Naye akaniambia: "Hawa ndio wale wanaotoka katika ile dhiki kuu,ⁱ nao wamefua kanzu zao na kuzifanya nyeupe katika damu ya Mwanakondoo.^j **15** Ndiyo sababu wako mbele ya kile kiti cha ufalme cha Mungu, nao wanamtolea utumishi mtakatifu mchana na usiku katika hekalu lake; na Yule anayeketi kwenye kiti cha ufalme^k atata ndaza hema lake juu yao.^l

SURA YA 7

a Isa 2:2
Ufu 15:4

b Ufu 7:14

c Law 23:40
Yoh 12:13

d Ufu 4:2, 3

e Mdo 4:12
Ufu 5:6

f Ufu 4:4
Ufu 11:16

g Ufu 4:11

h Ufu 7:9

i Mt 24:21
Mk 13:19

j Yoh 1:29
Ebr 9:14
1Yo 1:7
Ufu 1:5

k Ufu 4:2

l Zb 15:1
Ufu 21:3

Safu ya 2

a Zb 121:6
Isa 49:10

b Ufu 5:6

c Yoh 10:11

d Ufu 22:1

e Isa 25:8
Ufu 21:4

SURA YA 8

f Ufu 6:1

g Ufu 5:1

h Ufu 15:1

i Kut 30:1, 3

j Ufu 5:8

k Ufu 9:13

l Zb 141:2
Lu 1:10

m Kut 19:16
Ufu 4:5

n Ufu 8:7, 8
Ufu 8:10, 12
Ufu 9:1, 13
Ufu 11:15

o Ufu 16:2

16 Hawatakuwa na njaa wala kiu tena, wala jua halitawachoma wala joto lolote lenye kuunguza,^a **17** kwa sababu Mwanakondoo,^b aliye katikati ya kile kiti cha ufalme, atawachunga^c na kuwaongoza kwenye chemchemi za maji* ya uzima.^d Na Mungu atafuta kila chozi katika macho yao."^e

8 Alipofungua^f muhuri wa saba,^g kukawa na kimya mbinguni kwa karibu nusu saa. **2** Nami nikawaona wale malaika saba^h wanaosimama mbele za Mungu, nao wakape-wa tarumbeta saba.

3 Malaika mwingine, akiwa ameshika chombo cha uvumba* cha dhahabu,ⁱ akafika na kusimama kwenye madhabahu, naye akapewa kiasi kikubwa cha uvumba^j ili autoe pamoja na sala za watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu^k ambayo ilikuwa mbele ya kile kiti cha ufalme. **4** Moshi wa uvumba kutoka kwenye mkono wa huyo malaika ukapanda pamoja na sala^l za watakatifu mbele za Mungu. **5** Lakini mara moja malaika huyo akachukua kile chombo cha uvumba, akakijaza moto kutoka kwenye madhabahu na kukitupa duniani. Kukatokea ngurumo na sauti na radi^m na tetemeko la ardhi. **6** Na wale malaika saba wenyet tarumbeta sabaⁿ wakajitarisha kuzipiga.

7 Malaika wa kwanza akai-piga tarumbeta yake. Kuka-wa na mvua ya mawe na moto uliochanganyika na damu, nao ukatupwa duniani;^o

7:17 *Au "mabubujiko ya maji." 8:3

*Au "chetezo."

na theluthi moja ya dunia ikateketezwa, na theluthi moja ya miti ikateketezwa, na mimea yote mibichi ikateketezwa.^a

8 Malaika wa pili akaipiga tarumbeta yake. Na kitu fulani kama mlima mkubwa unao-waka moto kikatupwa ndani ya bahari.^b Na theluthi moja ya bahari ikawa damu;^c **9** na theluthi moja ya viumbe hai* wa baharini wakafa,^d na theluthi moja ya meli zikaharibiwa.

10 Malaika wa tatu akaipiga tarumbeta yake. Na nyota kubwa inayowaka kama taa ikaa-nguka kutoka mbinguni, ikaa-nguka juu ya theluthi moja ya mito na juu ya chemchemi za maji.^e **11** Jina la nyota hiyo ni Pakanga. Na theluthi moja ya maji ikageuka kuwa pakanga, na wanadamu wengi wakafa kutokana na maji hayo, kwa sababu yaligeuka kuwa machungu.^f

12 Malaika wa nne akaipiga tarumbeta yake. Na theluthi moja ya jua ikapigwa,^g pia theluthi moja ya mwezi, na theluthi moja ya nyota, ili theluthi moja ya hizo itiwie giza^h na mchana usiwe na nuru kwa theluthi moja, na usiku vivyo hivyo.

13 Nami nikaona na kusikia tai akiruka katikati ya mbingu akisema kwa sauti kubwa: "Ole, ole, ole" wao wanaokaa duniani kwa sababu ya milio mingine ya tarumbeta za wale malaika watatu walio karibu kuzipiga tarumbeta zao!^j

9 Malaika wa tano akaipiga tarumbeta yake.^k Nami nikaona nyota iliyokuwa imea-nguka kutoka mbinguni mpa-

8:9 *Au "viumbe wenye nafsi." 8:10 *Au "mabubujiko ya maji."

SURA YA 8

a Kut 9:23-25
Zb 97:3, 5

b Isa 17:12, 13
Isa 57:20

c Kut 7:20

d Ufu 16:1, 3

e Ufu 16:1, 4

f Amo 5:7

g Ufu 16:1, 8

h Kut 10:22

i Ufu 9:12
Ufu 11:14

j Ufu 8:2

SURA YA 9

k Ufu 8:2

Safu ya 2

a Lu 8:30, 31
Ufu 9:11
Ufu 20:1-3

b Yoe 2:2, 10

c Kut 10:12

d Ufu 7:2, 3

e Ufu 9:10

f Yoe 2:4, 5

g Yoe 1:6

h Yoe 2:4, 5

i Ufu 9:5

ka duniani, naye akapewa ufunguo wa shimo refu lisilo na mwisho.^{*a} **2** Akalifungua shimo refu lisilo na mwisho,^{*} na moshi ukapanda kutoka katika lile shimo kama moshi wa tanuru kubwa, na jua likatiwa giza,^b pia hewa, kwa moshi wa lile shimo. **3** Na nzi-ge wakatoka katika moshi huo wakaja duniani,^c nao wakapewa mamlaka, mamlaka kama ile ya nge wa dunia. **4** Wakaambiwa wasidhuru majani ya dunia au mmea wowote au mti wowote, isipokuwa watu wasio na muhuri wa Mungu kwenye mapaji ya nyuso zao.^d

5 Na nzi-ge hao walipewa ruhusa, si ya kuwaua, bali ya kuwatesa kwa miezi mitano, na mateso yao yalikuwa kama mateso ya mtu anapoumwa na nge.^e **6** Katika siku hizo watu watatafuta kifo lakini hawatakipata kamwe, nao watatamani kufa, lakini kifo kitatakimbia.

7 Wale nzi-ge walionekana kama farasi waliotayarishwa kwa ajili ya vita;^f na juu ya vichwa vyao kulikuwa na kitu kilichoonekana kama mataji ya dhahabu, na nyuso zao zilikuwa kama nyuso za wanadamu, **8** lakini walikuwa na nywele kama nywele za wanawake. Na meno yao yalikuwa kama ya simba,^g **9** nao walikuwa na mabamba ya kifuani kama mabamba ya kifuani ya chuma. Na sauti ya mabawa yao ilikuwa kama sauti ya magari ya farasi yakikimbia kwenda vitani.^h **10** Pia, wana mikia yenye miiba kama nge, na katika mikia yao wana mamlaka ya kuumiza watu kwa miezi mitano.ⁱ

9:1, 2 *Au "abiso." Angalia Kamusi, uku. 2012.

11 Wana mfalme juu yao, yule malaika wa shimo refu lisilo na mwisho.*^a Katika Kiebrania jina lake ni Abadoni,[#] lakini katika Kigiriki jina lake ni Apolioni.^Δ

12 Ole mmoja umepita. Tazama! Ole mbili zaidi^b zinakuja baada ya mambo haya.

13 Malaika wa sita^c akaipiga tarumbeta yake.^d Nami nikasikia sauti moja kutoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu^e iliyo mbele za Mungu **14** ikimwambia malaika wa sita aliyekuwa na tarumbeta: "Wafungue malaika wanne waliofungwa kwenye mto mkubwa Efrati."^f **15** Na wale malaika wanne, ambao wametayarishwa kwa ajili ya ile saa na siku na mwezi na mwaka wakafunguliwa ili waue theluthi moja ya watu.

16 Idadi ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa maku mi mawili ya maelfu ya maku mi ya maelfu;* niliisikia idadi yao. **17** Na hivi ndivyo nilivyowaona wale farasi katika maono na wale walioketi juu yao: Walikuwa na mabamba ya kifua ni ya rangi nyekundu ya moto na ya bluu ya hayasinthi na ya manjano ya kiberiti, na vichwa vya wale farasi vilikuwa kama vichwa vya simba,^g na moto na moshi na kiberiti vilitoka katika vinywa vyao. **18** Theluthi moja ya watu iliuawa kwa hayo mapigo matatu, kwa ule moto na moshi na kiberiti vilivyotoka katika vinywa vyao. **19** Kwa maana mam-

9:11 *Au "abiso." Angalia Kamusi, uku. 2012. #Maana yake "Uharibifu."
^ΔMaana yake "Mwangamizaji." 9:16 *Au "20,000 mara 10,000," yaani, 200,000,000.

SURA YA 9

a Ufu 9:1
Ufu 20:1-3

b Ufu 8:13

c Ufu 8:6

d Ufu 11:15

e Ufu 8:3

f Ufu 16:1,12
Ufu 17:1,15

g Met 28:1

Safu ya 2

a Zb 115:4-7

SURA YA 10

b Mt 17:1,2

c Ufu 5:5

d Kut 19:16
Ufu 4:5
Ufu 11:19

e Ufu 10:8

laka ya wale farasi imo katika vinywa vyao na katika mikia yao, kwa maana mikia yao ni kama nyoka na ina vichwa, nao wanaitumia kudhuru.

20 Lakini watu waliobaki ambao hawakuuawa kwa wale mapigo hawakutubu matendo ya mikono yao; hawakuacha kuabudu roho waovu na sanamu za dhahabu na fedha na shaba na mawe na miti, ambazo haziwezi kuona wala kusikia wala kutembea.^a **21** Nao hawakutubu mauaji yao wala mazoea yao ya kuwasiliana na roho wala uasherati* wao wala wizi wao.

10 Nami nikamwona malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, akiwa amepambwa* wingu, na upinde wa mvua ulikuwa juu ya kichwa chake, na uso wake ulikuwa kama jua,^b na miguu yake ilikuwa kama nguzo za moto, **2** na mkononi mwake alikuwa na kitabu kidogo cha kukunjwa kilichofunguliwa. Naye akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, na mguu wa kushoto juu ya dunia, **3** naye akapaza sauti kubwa kama simba anaponguruma.^c Na alipopaza sauti, sauti za zile ngurumo saba^d zikazungumza.

4 Basi zile ngurumo saba zilipozungumza, nilikuwa karibu kuandika; lakini nikasikia sauti kutoka mbinguni^e ikisema: "Yatie muhuri mambo ambayo zile ngurumo saba zilisema, nawe usiyaandike." **5** Malaika niliyemwona amesimama juu ya bahari na juu ya dunia akainua mkono wake

9:21 *Neno la Kigiriki, *por-ne'ra*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 10:1 *Au "amefunikwa."

wa kuume kuelekea mbinguni, **6** naye akaapa kwa Yule anayeishi milele na milele,^a aliyeiumba mbingu na vitu vilivyo ndani yake na dunia na vitu vilivyo ndani yake na bahari na vitu vilivyo ndani yake.^b “Hakuna kukawia tena. **7** Lakini katika siku ambazo yule malaika wa saba^c atakuwa karibu kuipiga tarumbeta yake,^d ile siri takatifu^e ambayo Mungu aliwatangazia ikiwa habari njema watumwa wake manabii^f itamalizika.”

8 Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni^g ikisema nami tena na kuniambia: “Nenda, ukichukue kile kitabu cha kukunjwa kilichofunguliwa, kilicho mkononi mwa malaika ambaye amesimama juu ya bahari na juu ya dunia.”^h **9** Nikaenda kwa yule malaika na kumwambia anipe kile kitabu kidogo cha kukunjwa. Akaniambia: “Kichukue ukile,ⁱ nacho kitafanya tumbo lako liwe na uchungu, lakini kinywani mwako kitakuwa kitamu kama asali.” **10** Nikakichukua kile kitabu kidogo cha kukunjwa kutoka mkononi mwa yule malaika nikakila,^j na kinywani mwangu kilikuwa kitamu kama asali,^k lakini baada ya kukila, tumbo langu likawa na uchungu. **11** Nao wakaniambia: “Lazima utoe unabii tena kuhusu jamii na mataifa na lugha na wafalme wengi.”

11 Nami nikapewa utete unaofanana na fimbo,^{*} nikaambiwa: “Simama upime patakatifu pa hekalu la Mungu na madhabahu na wale wanaoabudu ndani yake. **2** Lakini kuhusu ua ulio nje ya

11:1 *Au “fimbo ya kupimia.”

SURA YA 10

a Zb 90:2
Ufu 4:9

b Kut 20:11
Ne 9:6
Zb 146:6

c Ufu 8:6

d Ufu 11:15

e Mk 4:11

f Amo 3:7

g Ufu 10:4

h Ufu 10:1, 2

i Eze 2:8

j Yer 15:16

k Zb 119:103
Eze 3:1-3

SURA YA 11

l Eze 40:3

Safu ya 2

a Ufu 21:2

b Ufu 13:5

c Zek 4:3, 11

d Zek 4:12
Mt 5:14

e Zek 4:14

f Lu 4:25

g Ifa 17:1
Yak 5:17

h Kut 7:19

i Ufu 12:17
Ufu 13:7

j Ufu 11:11

patakatifu pa hekalu, uache wala usiupime, kwa sababu umepewa mataifa, nao watalikanyaga lile jiji takatifu^a chini ya miguu yao kwa miezi 42.^b **3** Nitawafanya mashahidi wangu wawili watoe unabii kwa siku 1,260 wakiwa wamevaa nguo za magunia.” **4** Hao wanafananishwa na ile mizeituni^c miwili na vile vinara viwili vya taa,^d na wamesimama mbele za Bwana wa dunia.^e

5 Yeyote akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vyao na kuwateketeza adui zao. Hivyo ndivyo anavyopaswa kuuawa mtu yeyote anayetaka kuwadhuru. **6** Hawa wana mamlaka ya kufunga anga^{*f} ili mvua isinyeshe^g katika siku zao za kutoa unabii, nao wana mamlaka juu ya maji ili kuyageuza kuwa damu^h na kuipiga dunia kwa kila aina ya mapigo mara nyingi wapendavyo.

7 Watakapomaliza kutoa ushahidi, yule mnyama wa mwituni anayepanda kutoka katika shimo refu lisilo na mwisho^{*} atapigana nao na kuwashinda na kuwaua.ⁱ **8** Na maiti zao zitakuwa kwenye barabara kuu ya lile jiji kubwa ambalo katika maana ya kiroho linaitwa Sodoma na Misri, ambako pia Bwana wao aliua wanao kwenye mti. **9** Na watu wa jamii na makabila na lugha na mataifa watazitamama maiti zao kwa siku tatu na nusu,^j wala hawataruhusu maiti zao zilazwe kaburini. **10** Na wale wanaokaa duniani wanashangilia juu yao na kusherehekea, nao watatumiana zawadi, kwa sababu hao manabii wa-

11:6 *Au “mbingu.” 11:7 *Au “abiso.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

wili waliwatesa watu wanao-
kaa duniani.

11 Baada ya zile siku tatu na nusu, roho ya uhai kuto-
ka kwa Mungu ikaingia nda-
ni yao,^a wakasimama kwa
miguu yao, na woga mkubwa
ukawaingia wale waliowaona.

12 Nao wakasikia sauti kubwa
kutoka mbinguni ikiwaambia:
"Pandeni mje huku." Nao wa-
kapanda kuingia mbinguni ka-
tika wingu, na adui zao wa-
kawaona.* **13** Tetemeko ku-
bwa la ardhi likatokea saa
hiyo, na sehemu ya kumi ya jiji
ikaanguka; na watu 7,000 wa-
kauawa na tetemeko hilo la
ardhi, na wale wengine wakawa
na hofu na kumpa utukufu
Mungu wa mbinguni.

14 Ole wa pili^b umepita. Ta-
zama! Ole wa tatu unakuja
upesii.

15 Malaika wa saba akaipi-
ga tarumbeta yake.^c Na sau-
ti kubwa zikasikika mbinguni,
zikisema: "Ufalme wa ulimwe-
ngu umekuwa Ufalme wa Bwa-
na wetu^d na wa Kristo wake,^e
naye atatawala akiwa mfalme
milele na milele."^f

16 Na wale wazee 24^g walio-
kuwa wameketi kwenye viti
vyao vya ufalme mbele za
Mungu wakaanguka kifudi-
fudi na kumwabudu Mungu,
17 wakisema: "Tunakushuku-
ru wewe, Yehova* Mungu,
Mweza-Yote, yule aliyeko^h na
aliyekuwako, kwa sababu ume-
chukua nguvu zako kuu na
kuanza kutawala ukiwa mfal-
me.ⁱ **18** Lakini mataifa waka-
wa na ghadhabu, nayo gha-
dhabu yako mwenyewe ikaja,
na wakati uliowekwa ukafika

11:12 *Au "walikuwa wakiwatazama."
11:17 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 11

a Eze 37:5, 10

b Ufu 9:12

c Ufu 8:6

d 1Nya 29:11
Zb 22:28
Da 4:17, 34
Ufu 12:10e Zb 2:6
Da 7:13, 14
Lu 1:32, 33
Lu 22:28, 29
2Pe 1:11f Zb 145:13
Da 2:44

g Ufu 4:10

h Ufu 1:4
Ufu 16:5i Zb 99:1
Zek 14:9
Ufu 19:6

Safu ya 2

a Ebr 11:6

b Amo 3:7
Ebr 1:1
Yak 5:10

c Mwa 6:11

d 1Fa 8:1, 6
Ebr 8:1, 2
Ebr 9:11

SURA YA 12

e Mwa 3:15

f Ufu 12:9
Ufu 20:2

g Ayu 38:7

h Mwa 6:2
Yud 6

i Mwa 3:15

j Ufu 11:15

k Zb 2:9
Zb 110:2
Ufu 19:15

kwa ajili ya kuhukumiwa kwa
wafu na kuwapa thawabu^a wa-
tumwa wako manabii^b na wa-
takatifu na wale wanaoliogo-
pa jina lako, wadogo kwa wa-
kubwa, na kuwaharibu wale
wanaoiharibu dunia."^{*c}

19 Na patakatifu pa heka-
lu la Mungu palipo mbinguni
pakafunguliwa, na sanduku la
agano lake likaonekana kati-
ka patakatifu pa hekalu lake.^d
Na kukatokea radi na sauti na
ngurumo na tetemeko la ardhi
na mvua kubwa ya mawe.

12 Kisha ishara kubwa
ikaonekana mbinguni:
Mwanamke^e aliyepambwa*
juu, na mwezi ulikuwa chini ya
miguu yake, na juu ya kichwa
chake palikuwa na taji la nyota
12, **2** naye alikuwa na mi-
mba. Na alikuwa akilia akiwa
katika maumivu na uchungu
wa kuzaa.

3 Ishara nyingine ikaoneka-
na mbinguni. Tazama! Joka
mkubwa wa rangi ya moto,^f
mwenye vichwa saba na pem-
be kumi na mataji saba* juu
ya vichwa vyake; **4** na mkia
wake unakokota theluthi moja
ya nyota^g za mbinguni, naye
akazitupa chini duniani.^h Na
huyo joka akaendelea kusi-
mama mbele ya yule mwanam-
mkeⁱ aliyekuwa karibu kuzaa,
ili atakapozaa, ammeze mto-
to wake.

5 Na yule mwanamke aka-
zaa mwana,^j wa kiume, ata-
kayeचना mataifa yote
kwa fimbo ya chuma.^k Na mto-
to wake akanyakuliwa* mpa-
ka kwa Mungu na kwenye kiti

11:18 *Au "kuwaangamiza wale wa-
naoangamiza dunia." 12:1 *Au "ali-
yevikwa." 12:3 *Au "tepe saba za
kichwani za kifalme." 12:5 *Au "aka-
chukuliwa."

chake cha ufalme. **6** Na yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotayarishwa na Mungu, na hapo watamlisha kwa siku 1,260.^a

7 Na vita vikatokea ghafla mbinguni: Mikaeli^{*b} na malai-ka zake wakapigana na yule joka, naye joka na malaika zake wakapigana nao **8** lakini hawakushinda,^{*} wala mahali hapakupatikana tena mbinguni kwa ajili yao. **9** Basi yule joka mkubwa^c akatupwa chini, yule nyoka wa zamani,^d anayeitwa Ibilisi^e na Shetani,^f anayeipotosha dunia nzima inayokaliwa;^g akatupwa chini duniani,^h na malaika zake wakatupwa chini pamoja naye. **10** Nikasikia sauti kubwa mbinguni ikisema:

“Sasa kumekuwa na wokovu/ na nguvu na Ufalme wa Mungu wetu/ na mamlaka ya Kristo wake, kwa sababu mshtaki wa ndugu zetu ametupwa chini, anayewashtaki mchana na usiku mbele za Mungu wetu!^k

11 Nao wakamshinda/ kwa sababu ya damu ya Mwanakondoo^m na kwa sababu ya neno lao la kutoa ushahidi,ⁿ nao hawakupenda nafsi zao^o hata walipokabili kifo. **12** Kwa sababu hiyo furahini, enyi mbingu nanyi mnaokaa ndani yake! Ole wa dunia na wa bahari,^p kwa sababu Ibilisi ameshuka kwenu, akiwa na hasira kali, akijua kwamba ana kipindi kifupi cha wakati.”^q

13 Sasa yule joka alipoona kwamba ametupwa chini duniani,^r alimtesa yule mwanamke^s aliyeezaa mtoto wa kiu-

12:7 *Maana yake “Ni Nani Aliye Kama Mungu?” **12:8** *Au labda, “lakini alishindwa [yaani, joka].” **12:11** *Au “uhai wao.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

SURA YA 12

a Ufu 12:14

b Da 10:13
Da 12:1
Yud 9c Ufu 12:3
Ufu 20:2d Mwa 3:1
2Ko 11:3
Ufu 12:14e Mt 4:1
Yoh 8:44
Ebr 2:14
Yak 4:7
1Pe 5:8f 1Nya 21:1
Ayu 1:6
Zek 3:2
Mt 4:10
Yoh 13:27
Ro 16:20
2Th 2:9g 2Ko 4:4
2Ko 11:14
Efe 2:2
1Yo 5:19h Lu 10:18
Ufu 12:13i Ro 13:11
Ebr 9:28
1Pe 1:5

j Ufu 11:15, 17

k Ayu 1:9
Zek 3:1

l 1Yo 2:14

m 1Pe 1:18, 19

n Mdo 1:8
2Ti 1:8
Ufu 1:9o Mt 16:25
Lu 14:26
Mdo 20:24p Isa 57:20
Isa 60:2
Ufu 17:15q Mt 24:34
Ro 16:20
2Ti 3:1
2Pe 3:3

r Lu 10:18

s Mwa 3:15
Ufu 12:1

Safu ya 2

a Kut 19:4
Isa 40:31

b Ufu 12:6

c Mwa 3:1

d 2Ko 11:3

e Mwa 3:15

f Mt 24:9

g Mdo 1:8

h Ufu 1:9

i Ufu 6:9

SURA YA 13

f Ufu 11:7

g Ufu 13:18

h Isa 57:20

i Ufu 21:1

j Ufu 12:9

k Lu 4:6

me. **14** Lakini yule mwanamke akapewa mabawa mawili ya tai mkubwa,^a ili aruke kwenda nyikani mahali pake, ambapo atalishwa kwa wakati na nyakati na nusu ya wakati^{*b} mbali na uso wa yule nyoka.^c

15 Naye nyoka akatapika maji kama mto kutoka katika kinywa chake nyuma ya yule mwanamke, ili kumzamisha katika mto huo. **16** Lakini dunia ikaja kumsaidia mwanamke, nayo dunia ikafungua kinywa chake na kuumeza mto ambao yule joka aliutapika kutoka katika kinywa chake.

17 Basi yule joka akawa na ghadhabu kumwelekea yule mwanamke, naye akaenda zake kupigana na wale walio-baki wa uzao wake,^{*d} wanaoshika amri za Mungu na walio na kazi ya kutoa ushahidi kumhusu Yesu.^e

13 Naye^{*} akasimama tuli juu ya mchanga wa bahari.

Nami nikamwona mnyama wa mwituni^f akipanda kutoka baharini,^g naye alikuwa na pembe kumi na vichwa saba, na mataji kumi^h juu ya pembe zake, lakini juu ya vichwa vyake majina yenye makufuru. **2** Basi yule mnyama wa mwituni niliyemwona alikuwa kama chui, lakini miguu yake ilikuwa kama ya dubu, na kinywa chake kilikuwa kama kinywa cha simba. Na yule joka^h akampa huyo mnyama nguvu zake na kile kiti chake cha ufalme na mamlaka kubwa.ⁱ

12:14 *Yaani, nyakati tatu na nusu. **12:17** *Tnn., “mbegu yake.” **13:1** *Yaani, yule joka. [#]Au “tepe kumi za kichwani za kifalme.”

3 Nikaona kimoja kati ya vichwa vyake kikiwa kimejeruhiwa vibaya lakini jeraha hilo la kifo lilipona,^a na dunia yote ikamfuata kwa mshangao yule mnyama wa mwituni. 4 Nao wakamwabudu yule joka kwa sababu alimpa mamlaka yule mnyama wa mwituni, nao wakamwabudu mnyama wa mwituni kwa maneno haya: "Ni nani aliye kama huyu mnyama wa mwituni, na ni nani anayeweza kupigana naye?"

5 Akapewa kinywa kinachosema mambo makuu na makufuru, akapewa pia mamlaka ya kutenda kwa miezi 42.^b

6 Naye akafungua kinywa chake kwa kumkufuru.^c Mungu ili kulikufuru jina lake na makao yake, na hata wale wanaokaa mbinguni.^d 7 Akapewa ruhusa ya kupigana vita na watakatifu na kuwashinda,^e na akapewa mamlaka juu ya kila kabila na watu na lugha na taifa. 8 Na wale wote wanaokaa duniani watamwabudu. Tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu, hakuna jina la hata mmoja wao lililoandikwa katika kitabu cha kukunjwa cha uzima^f cha Mwanakondoo aliyechinjwa.^g

9 Ikiwa yeyote ana sikio, na asikie.^h 10 Ikiwa yeyote amekusudiwa kwenda utekwani, ataenda utekwani. Ikiwa yeyote ataua* kwa upanga, naye lazima auawe kwa upanga.ⁱ Hapa ndipo watakatifu/ wanahitaji uvumilivu^k na imani.^l

11 Kisha nikamwona mnyama mwingine wa mwituni aki-panda kutoka katika dunia, naye alikuwa na pembe mbi-li kama mwanakondoo, laki-

13:10 *Au labda, "Ikiwa yeyote atalazimika kuuawa."

SURA YA 13

a Ufu 13:14

b Ufu 11:2, 3

c Da 7:25

d Ufu 12:12

e Ufu 12:17

f Ufu 3:5
Ufu 21:27g Isa 53:7
Mt 27:50
Ufu 5:6, 12

h Mt 11:15

i Mt 26:52

j Da 7:18
1Ko 6:2
Ufu 20:6k Mt 24:13
Ebr 10:36
Ebr 12:3

l Ufu 2:10

Safu ya 2

a Ufu 16:13
Ufu 20:2

b Ufu 13:1

c Ufu 13:3

d Ufu 19:20
Ufu 20:4

e Ufu 13:3

f Ufu 14:9, 10
Ufu 16:2
Ufu 19:20

g Ufu 14:11

h Ufu 15:2

i Da 3:1

ni akaanza kuzungumza kama joka.^a 12 Anatumia mamlaka yote ya yule mnyama wa kwanza wa mwituni^b aliye machoni pake. Naye huifanya dunia na wale wanaokaa duniani wamwabudu yule mnyama wa kwanza wa mwituni, ambaye jeraha lake la kifo lilipona.^c 13 Naye hufanya ishara kubwa, hata hufanya moto ushuke kutoka mbinguni mpa-ka duniani machoni pa wanaadamu.

14 Naye huwapotosha wale wanaokaa duniani, kwa sababu ya ishara alizoruhusiwa kufanya machoni pa yule mnyama wa mwituni, huku akiwambia wale wanaokaa duniani watengeneze sanamu^d ya yule mnyama wa mwituni aliyekuwa na pigo la upanga lakini bado akabaki hai.^e 15 Naye akaruhusiwa kuipa pumzi* ile sanamu ya mnyama wa mwituni, ili ile sanamu ya mnyama wa mwituni iweze kusema na pia kufanya wale wote wanaokataa kuiabudu ile sanamu ya mnyama wa mwituni wauawe.

16 Anawalazimisha watu wote—wadogo kwa wakubwa, matajiri kwa maskini, walio huru kwa watumwa—ili wote watiwe alama kwenye mkono wao wa kulia au kwenye paji la uso wao,^f 17 na ili yeyote asiweze kununua au kuuza isipokuwa mtu aliye na ile alama, jina^g la yule mnyama wa mwituni au namba ya jina lake.^h 18 Hapa ndipo hekima inapohitajiwa: Yule aliye na ufahamu na afanye hesabu ya namba ya yule mnyama wa mwituni, kwa maana ni namba ya mwanadamu, na namba yake ni 666.ⁱ

13:15 *Au "roho."

14 Kisha nikaona, na tazama! Mwanakondoo^a amesimama juu ya Mlima Sanyuni,^b na pamoja naye 144,000^c walioandikwa jina lake na jina la Baba yake^d kwenye mapaji ya nyuso zao. **2** Nikasikia sauti kutoka mbinguni kama sauti ya maji mengi na kama sauti ya ngurumo kubwa; na sauti niliyosikia ilikuwa kama ya wambaji wanao-
fuatanisha sauti zao wakipiga vinubi vyao. **3** Nao wanaimba kana kwamba ni wimbo mpya^e mbele ya kile kiti cha ufalme na mbele ya wale viumbe hai wanne^f na wale wazee,^g na hakuna yeyote aliyeweza kujifunza kika-
mili wimbo ule ila wale 144,000,^h ambao wamenunuliwa kutoka duniani. **4** Hao ndio wale ambao hawakujitia unajisi na wanawake; kwa kweli, wao ni mabikira.ⁱ Hao ndio wanaoendelea kumfuata Mwanakondoo popote anapoenda.^j Hao walinunuliwa^k kutoka kati ya wanadamu wakiwa matunda ya kwanza^l kwa Mungu na kwa Mwanakondoo, **5** na hamna udanganyifu uliopatikana katika vinywa vyao; wao hawana dosari.^m

6 Nami nikamwona malaika mwingine akiruka katikati ya mbingu,^{*} naye alikuwa na habari njema ya milele ili aita-
ngaze kwa wale wanaokaa duniani, kwa kila taifa na kabila na lugha na watu.ⁿ **7** Alikuwa akisema kwa sauti kubwa: “Mwogopeni Mungu na kumpa utukufu, kwa sababu saa ya hukumu yake imefika,^o kwa hiyo mwabuduni Yule aliyeziumba mbingu na dunia

14:6 *Au “katikati ya anga; juu.”

SURA YA 14

a Yoh 1:29

Ufu 5:6

Ufu 22:3

b Zb 2:6

Ebr 12:22

1Pe 2:6

c Ufu 7:4

d Ufu 3:12

e Zb 33:3

Zb 98:1

Zb 149:1

Ufu 5:9

f Ufu 4:6

g Ufu 4:4

Ufu 19:4

h Ufu 7:4

i 2Ko 11:2

Yak 1:27

Yak 4:4

j 1Pe 2:21

k 1Ko 6:20

1Ko 7:23

Ufu 5:9

l Yak 1:18

m Efe 5:25-27

Yud 24

n Mt 24:14

Mk 13:10

Mdo 1:8

o 2Pe 2:9

Safu ya 2

a Kut 20:11

Zb 146:6

b Ufu 17:18

c Isa 21:9

Ufu 18:21

d Yer 51:7,8

Ufu 17:1, 2

Ufu 18:2, 3

e Ufu 13:1

f Ufu 13:15, 16

g Zb 75:8

Ufu 11:18

Ufu 16:19

h Ufu 21:8

i Mt 25:46

2Th 1:9

Ufu 19:3

j Ufu 13:16-18

Ufu 16:2

Ufu 20:4

k Ufu 13:10

l Ebr 10:38

m 1Ko 15:51, 52

1Th 4:16, 17

na bahari^a na chemchemi za maji.”*

8 Na mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema: “Ameanguka! Babiloni Mku-bwa^b ameanguka,^c yule aliye-yafanya mataifa yote yanywe divai ya hamu* ya uasherati[#] wake!”^d

9 Malaika mwingine, wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kubwa: “Yeyote akimwabudu yule mnyama wa mwituni^e na sanamu yake na kupokea alama kwenye paji la uso wake au kwenye mko-
no wake,^f **10** yeye pia ataku-
nywa divai ya hasira ya Mungu inayomwagwa ndani ya kiko-
mbe cha ghadhabu Yake bila kuchanganywa na kitu,^g naye atateswa kwa moto na kibe-
riti^h machoni pa malaika wa-
takatifu na machoni pa Mwa-
nakondoo. **11** Na moshi wa kuteswa kwao unapanda mi-
lele na milele,ⁱ nao hawana pu-
mziko mchana na usiku, wale wanaomwabudu yule mnyama wa mwituni na sanamu yake na yeyote anayepokea alama ya jina lake.^j **12** Hapa ndipo watakatifu wanapohitaji uvu-
milivu,^k wale wanaoshika amri za Mungu na kushika imara imani^l kwa Yesu.”

13 Nami nikasikia sauti kuto-
ka mbinguni ikisema, “Andi-
ka: Wenye furaha ni wafu wa-
naokufa katika muungano na Bwana^m tangu wakati huu na kuendelea. Ndiyo, roho inase-
ma, acheni wapumzike kuto-
kana na kazi yao ngumu, kwa maana mambo waliyotenda yanaambatana nao moja kwa moja.”*

14:7 *Au “mabubujiko ya maji.” 14:8 *Au “hasira.” #Neno la Kigiriki, *por-nei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. 14:13 *Au “pamoja nao.”

14 Kisha nikaona, na tazama! wingu jeupe, na mtu fulani kama mwana wa binadamu alikuwa ameketi juu ya wingu hilo,^a akiwa na taji la dhahabu juu ya kichwa chake na mundu mkali mkononi mwake.

15 Malaika mwingine akatokea katika patakatifu pa hekalu, akimwambia kwa sauti kubwa yule aliyeketi juu ya lile wingu: "Tia ndani mundu wako uvune, kwa sababu saa ya kuvuna imefika, kwa maana mavuno ya dunia yameiva kabisa."^b **16** Na yule aliyeketi juu ya wingu akautia mundu wake duniani, nayo dunia ikavunwa.

17 Na bado malaika mwingine akatokea katika patakatifu pa hekalu palipo mbinguni, naye pia alikuwa na mundu mkali.

18 Na bado malaika mwingine akatokea katika madhabu naye alikuwa na mamla-ka juu ya moto. Naye akamwambia kwa sauti kubwa yule aliyekuwa na mundu mkali: "Tia ndani mundu wako mkali ukusanye vishada vya mزابibu wa dunia, kwa sababu mزابibu zake zimeiva."^c **19** Yule malaika akatia mundu wake katika dunia na kuukusanya mزابibu wa dunia, naye akautupa ndani ya shinikizo kubwa la divai la hasira ya Mungu.^d **20** Lile shinikizo la divai likakanyagiwa nje ya jiji, na damu ikatoka katika lile shinikizo la divai hata kufikia juu kwenye lijamu za farasi umbali wa stadia 1,600.*

14:20 *Karibu kilomita 296 (maili 184). Stadiumu moja ilikuwa sawa na mita 185 (futi 606.95). Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 14

a Da 7:13

b Mt 13:30

c Yoe 3:13

d Ufu 19:11, 15

Safu ya 2

SURA YA 15

a Ufu 16:1

b Ufu 16:17

c 1Fa 7:23
Ufu 4:6

d Ufu 2:7

e Ufu 13:15

f Ufu 13:18

g Kut 15:1
Kum 31:30

h Yoh 1:29

i Kut 15:11
Zb 111:2
Zb 139:14

j Kut 6:3

k Kum 32:4
Zb 145:17l Yer 10:10
ITI 1:17

m Yer 10:6, 7

n Zb 86:9
Mal 1:11o Mdo 7:44
Ebr 8:1, 2
Ebr 9:11

p Ufu 11:19

q Ufu 15:1

r Zb 75:8
Yer 25:15
Ufu 14:9, 10

15 Nami nikaona huko mbinguni ishara nyingine kubwa na ya ajabu sana, malaika saba^a wenye mapigo saba. Hayo ndiyo ya mwisho, kwa sababu kupitia hayo hasira ya Mungu inamalizika.^b

2 Nami nikaona kitu kama bahari ya kioo^c iliyochanganyika na moto, na wale wanaomshinda^d yule mnyama wa mwituni na sanamu yake^e na ile namba ya jina lake^f walikuwa wamesimama kando ya ile bahari ya kioo, wakiwa wameshika vinubi vya Mungu. **3** Walikuwa wanaimba wimbo wa Musa^g mtumwa wa Mungu na mima ya Mwanakondoo,^h wakisema:

"Matendo yako ni makuu na ya ajabu,ⁱ Yehova* Mungu, Mweza-Yote.^j Njia zako ni za uadilifu na za kweli,^k Mfalme wa umilele.^l **4** Ni nani ambaye kwa kweli hatakuogopa wewe, Yehova,* na kulitukuza jina lako, kwa kuwa wewe peke yako ni mshikamanifu?^m Kwa maana mataifa yote yatakuja na kuabudu mbele zako,ⁿ kwa sababu amri zako za uadilifu zimefunuliwa."

5 Baada ya hayo nikaona, patakatifu pa hema la ushahidi^o pakifunguliwa mbinguni,^p **6** na wale malaika saba wenye mapigo saba^q wakatokea katika patakatifu, wakiwa wamevaa kitani safi, kinachong'aa na wakiwa wamefunga mishiipi ya dhahabu kifuaani. **7** Mmoja wa wale viumbe hai wanne akawapa wale malaika saba mabakuli saba ya dhahabu yaliyojaa hasira ya Mungu,^r anayeishi milele na milele. **8** Na patakatifu pakajaa

15:3, 4 *Angalia Nyongeza A5.

moshi kwa sababu ya utukufu wa Mungu^a na kwa sababu ya nguvu zake, na hakuna yeyote aliyeweza kuingia patakatifu mpaka yale mapigo saba^b ya wale malaika saba yalipomalizika.

16 Nami nikasikia sauti kubwa kutoka katika patakatifu^c ikiwaambia wale malaika saba: "Nendeni mkamwaga yale mabakuli saba ya hasira ya Mungu juu ya dunia."^d

2 Malaika wa kwanza akaenda na kumwaga bakuli lake juu ya dunia.^e Na kidonda chenye maumivu na kilicho hatarifu^f kikawapata watu waliokuwa na alama ya yule mnyama wa mwituni^g na waliokuwa wakiiabudu sanamu yake.^h

3 Malaika wa pili akamwaga bakuli lake ndani ya bahari.ⁱ Nayo ikawa damu^j kama ya mwanadamu aliyekufa, na kila kiumbe aliyehai akafa,* ndiyo, vitu vilivyo ndani ya bahari.^k

4 Malaika wa tatu akamwaga bakuli lake ndani ya mito na chemchemi za maji.*^l Nazo zikawa damu.^m **5** Nikamsikia malaika aliyehai juu ya maji akisema: "Wewe, Amba- yame uko na uliyekuwako,ⁿ Mshikamanifu,^o wewe ni mwadilifu, kwa kuwa umetoa hukumu hizi,^p **6** kwa sababu waliimwaga damu ya watakatifu na ya manabii,^q nawe wanewapa damu wanywe;^r wanastahili hivyo."^s **7** Nikasikia madhabahu ikisema: "Ndiyo, Yehova* Mungu, Mweza-Yote,^t hukumu zako^u ni za kweli na za uadilifu."^u

16:3 *Au "kila nafsi ikafa." **16:4** *Au "mabubujiko ya maji." **16:7** *Angalia Nyongeza A5. ^aAu "maamuzi yako ya hukumu."

SURA YA 15

a Kut 40:34, 35
1Fa 8:10, 11
Isa 6:4
Eze 44:4

b Ufu 15:1

SURA YA 16

c Ufu 16:17

d Zb 69:24
Sef 3:8

e Ufu 8:7

f Kut 9:10

g Ufu 13:16, 18

h Ufu 13:15
Ufu 19:20

i Ufu 8:8

j Kut 7:20

k Isa 57:20

l Ufu 8:10

m Kut 7:20
Zb 78:44

n Ufu 1:4

o Zb 145:17
Ufu 15:4

p Kum 32:4
Zb 119:137

q Zb 79:3

r Isa 49:26

s Ufu 18:20

t Kut 6:3

u Zb 19:9
Zb 119:137
Ufu 19:1, 2

Safu ya 2

a Ufu 8:12

b Kut 10:21
Isa 8:22

c Ufu 9:13, 14

d Yer 50:38

e Isa 44:27, 28

f Ufu 12:3

g Ufu 13:11, 13

h Ufu 19:19

i Isa 13:6
Yer 25:33
Eze 30:3

Yoe 1:15

Yoe 2:1, 11

Sef 1:15

2Pe 3:11, 12

j 1Th 5:2

2Pe 3:10

k Lu 21:36

8 Malaika wa nne akamwaga bakuli lake juu ya jua,^a nalo jua likapewa ruhusa ya kuwaunguza watu kwa moto.

9 Na wale watu wakaunguzwa na joto hilo kali, lakini wakalikufuru jina la Mungu, aliye na mamlaka juu ya mapigo haya, nao hawakutubu wala kumpa utukufu.

10 Malaika wa tano akamwaga bakuli lake juu ya kiti cha ufalme cha yule mnyama wa mwituni. Na ufalme wake ukatiwa giza,^b nao wakaanza kuzitafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu yao,

11 lakini wakamkufuru Mungu wa mbinguni kwa sababu ya maumivu yao na vidonda vyao, nao hawakutubu mate- ndo yao.

12 Malaika wa sita akamwaga bakuli lake juu ya mto mku- bwa Efrati,^c na maji yake ya- kakauka^d ili kutayarisha njia kwa ajili ya wafalme^e wanao- toka mashariki.*

13 Nami nikaona maneno matatu machafu yaliyoongo- zwa na roho* ambayo yalioneka kama vyura yakitoka ka- tika kinywa cha yule mnyama wa mwituni na katika ki- nywa cha yule nabii wa uwongo. **14** Kwa kweli, hayo ni maneno yanayoongozwa na roho waovu nayo yanafanya ishara,^g nayo yanakwenda kwa wafalme wa dunia nzi- ma inayokaliwa, ili kuwakusanya pamoja kwa vita^h vya siku kuu ya Mungu Mweza-Yote.ⁱ

15 "Tazama! Ninakuja kama mwizi.^j Mwenye furaha ni yule anayekaa macho^k na kutunza

16:12 *Au "mawio ya jua." **16:13** *Tnn., "roho waovu."

mavazi yake ya nje, ili asijie akatembea uchi na watu wai-tazame aibu yake.”^a

16 Nayo yakawakusanya pa-moja mahali panapoitwa kati-ka Kiebrania Har-Magedoni.*^b

17 Malaika wa saba aka-mwaga bakuli lake juu ya hewa. Ndipo sauti kubwa ika-tokea katika patakatifu^c kwe-nye kile kiti cha ufalme, iki-sema: “Imetimia!” **18** Kuka-wa na radi na sauti na ngu-rumo, na kukatokea tetemeko kubwa la ardhi ambalo ha-lijawahi kutokea tangu wa-nadamu walipoubwa dunia-ni,^d tetemeko hilo la ardhi lili-kuwa kubwa sana na lilienea sana. **19** Lile jiji kubwa^e lika-pasuka na kuwa sehemu tatu, na majiji ya mataifa yakaa-nguka; na Babiloni Mkubwa^f akakumbukwa mbele za Mu-ngu, ili kumpa kikombe cha divai cha hasira ya ghadhabu yake.^g **20** Pia, kila kisiwa ki-katoweka, na milima haikupa-tikana tena.^h **21** Ndipo mvua kubwa ya mawe, kila jiwe liki-wa na uzito wa karibu talanta moja,* ikanyesha kutoka mbi-nguni juu ya watu,ⁱ nao watu wakamkufuru Mungu kwa sa-babu ya lile pigo la mvua ya mawe,^j kwa kuwa pigo hilo li-likuwa kubwa mno.

17 Mmoja wa wale malai-ka saba waliokuwa na mabakuli saba^k akaja na ku-niambia: “Njoo, nitakuonye-sha hukumu dhidi ya yule ka-haba mkubwa anayekaa juu ya maji mengi,^l **2** ambaye wafal-

16:16 *Neno la Kigiriki, *Har Ma-ge-don'*, kutokana na neno la Kiebrania lina-lomaanisha “Mlima wa Megido.” **16:21** *Talanta ya Kigiriki ilikuwa sawa na ki-logramu 20.4. Angalia Nyongeza B14.

SURA YA 16

a Ufu 3:18

b 2Nya 32:22
Zek 12:11
Ufu 19:19

c Ufu 16:1

d Eze 38:19
Da 12:1
Ebr 12:26

e Ufu 17:18

f Ufu 18:2

g Yer 25:15
Ufu 15:7

h Ufu 6:14

i Ayu 38:22, 23

j Kut 9:24

SURA YA 17

k Ufu 16:1

l Yer 51:13
Ufu 17:15
Ufu 19:2

Safu ya 2

a Yak 4:4
Ufu 18:9b Yer 51:7
Ufu 14:8
Ufu 18:3

c Lu 16:19

d Ufu 18:11, 12
Ufu 18:19

e Ufu 19:2

f Ufu 18:5

g Ufu 6:9
Ufu 18:24
Ufu 19:2

h Ufu 17:5

i Ufu 17:3

j Ufu 20:1

me wa dunia walifanya uasher-rati* naye,^a na watu wanaokaa duniani walileweshwa kwa di-vai ya uasherati[#] wake.”^b

3 Naye akanichukua kati-ka nguvu za roho akanipele-ka nyikani. Nami nikamwo-na mwanamke ameketi juu ya mnyama wa mwituni mwenye rangi nyekundu aliyejaa ma-jina ya makufuru na aliyeku-wa na vichwa saba na pembe kumi. **4** Yule mwanamke ali-kuwa amevaa nguo za rangi ya zambarau^c na nyekundu, naye alikuwa amepambwa kwa dha-habu na mawe ya thamani na lulu,^d na mkononi mwake ali-kuwa na kikombe cha dha-habu kilichojaa machukizo na mambo machafu ya uasher-rati[#] wake. **5** Kwenye paji la uso wake alikuwa amendi-kuwa jina la fumbo: “Babiloni Mkubwa, mama wa makaha-ba^e na wa machukizo ya du-nia.”^f **6** Nami nikaona kwa-mba yule mwanamke amelewa damu ya watakatifu na damu ya mashahidi wa Yesu.^g

Basi, nilipomwona nilisha-ngaa sana. **7** Ndipo yule ma-laika akaniambia: “Kwa nini ulishangaa? Nitakuambia fumbo la yule mwanamke^h na la yule mnyama wa mwituni anayembeba na aliye na vi-chwa saba na pembe kumi:ⁱ **8** Mnyama wa mwituni uliyemwona alikuwako, lakini hayu-ko, na bado yuko karibu kupanda kutoka katika shimo refu lisilo na mwisho,^{*j} naye ataenda kwenye uharibifu. Na watu wanaokaa du-niani ambao majina yao

17:2 *Angalia Kamusi, uku. 2012. **17:2, 4** *Neno la Kigiriki *pornef'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. **17:8** *Au “abiso.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

hayajaandikwa katika kitabu cha kukunjwa cha uzima^a tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu watahangaa watakapoona jinsi yule mnyama wa mwituni alivyokuwako, lakini hayuko, na bado atakuwapo.

9 "Hilo linahitaji akili yenye hekima: Vile vichwa saba^b vinamaanisha milima saba, ambapo yule mwanamke huketi juu yake. **10** Na kuna wafalme saba: Watano wameanguka, mmoja yuko, na yule mwingine bado hajafika; lakini atakapofika, lazima akae kwa muda mfupi. **11** Na yule mnyama wa mwituni aliyekuwako lakini hayuko,^c yeye pia ni mfalme wa nane, lakini anatokana na wale saba, naye anaenda zake kwenye uharibifu.

12 "Pembe kumi ulizoona zinamaanisha wafalme kumi ambao bado hawajapokea ufalme, lakini wanapokea mamlaka wakiwa wafalme kwa saa moja pamoja na yule mnyama wa mwituni. **13** Hao wana wazo moja, kwa hiyo wanampa yule mnyama wa mwituni nguvu na mamlaka yao. **14** Nao watapigana na Mwanakondoo,^d lakini kwa sababu yeye ni Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme,^e Mwanakondoo atawashinda.^f Pia, wale walio pamoja naye walioitwa na waliochaguliwa na walio waaminifu watawashinda."^g

15 Akaniambia: "Yale maji uliyoyaona, ambapo yule kahaaba ameketi, yanamaanisha jamii za watu na umati na mataifa na lugha.^h **16** Na zile pembe kumiⁱ ulizoona, na yule mnyama wa mwituni,^j hao watamchukia yule kahaaba^k na kumfanya kuwa uki-

SURA YA 17

a Kut 32:32
Zb 69:28
Flp 4:3

b Ufu 17:7

c Ufu 17:8

d Yoh 1:29
Ufu 5:6

e Mt 28:18
Mdo 2:36
1Ti 6:15

f Ufu 19:11, 15

g Ro 16:20

h Isa 57:20
Yer 51:13

i Ufu 17:12

j Ufu 17:8

k Ufu 17:7

Safu ya 2

a Law 21:9
Ufu 18:8

b Yos 11:19, 20
Met 21:1

c Ufu 17:12

d Ufu 17:5

SURA YA 18

e Isa 21:9
Yer 51:8
Ufu 14:8

f Isa 13:21
Yer 50:39

g Yer 51:7

h Ufu 17:1, 2

i Isa 48:20
Isa 52:11
Yer 50:8

j Yer 51:6, 45
2Ko 6:17

k Yer 51:9

wa na uchi, nao watakula nyama yake na kumteketeza kabisa kwa moto.^a **17** Kwa maana Mungu alitia hilo ndani ya mioyo yao ili kutekeleza wazo lake,^b ndiyo, kutekeleza lile wazo lao moja kwa kumpa yule mnyama wa mwituni^c ufalme wao, mpaka maneno ya Mungu yatakapokwisha kutimiza.^d **18** Na yule mwanamke^d uliyemwona anamaanisha lile jiji kubwa lililo na ufalme juu ya wafalme wa dunia."

18 Baada ya hayo nika mwona malaiika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kubwa, na dunia ikatiwa nuru kwa utukufu wake. **2** Naye akasema kwa sauti yenye nguvu: "Ameanguka! Babiloni Mku-bwa ameanguka,^e naye amekwa makao ya roho waovu na mahali pa kuvizia pa kila roho mchafu* na kila ndege mchafu anayechukiwa!^f **3** Kwa sababu ya divai ya hamu* ya uasherati^g wake, mataifa yote yamenaswa,^g na wafalme wa dunia walifanya uasherati naye,^h na wafanyabiashara^Δ wa dunia walikuwa matajiri kutokana na nguvu za anasa yake isiyo na aibu."

4 Nami nikasikia sauti nyengine kutoka mbinguni ikisema: "Tokeni kwake, watu wangu,ⁱ ikiwa hamtaki kushiriki pamoja naye dhambi zake, na ikiwa hamtaki kupokea sehemu ya mapigo yake.^j **5** Kwa maana dhambi zake zimekusanyika pamoja mpaka mbinguni,^k naye Mungu ame-

18:2 *Au labda, "pumzi chafu; maneno yaliyoongozwa na roho." **18:3** *Au "hasira." ^ΔNeno la Kigiriki *pornei'a*. Angalia Kamusi, uku. 2012. ^ΔAu "wafanyabiashara wanaosafiri."

kumbuka matendo yake yasiyo ya haki.*^a **6** Mlipeni kama alivyowatendea wengine,^b ndiyo, mlipeni mara mbili kwa yale aliyotenda;^c katika kiko-mbe^d alichochanganya, mtilieni mchanganyiko mara mbili.^e **7** Kwa kadiri alivyojikutuza na kuishi katika anasa isiyo na aibu, kwa kadiri hiyo mpeni mateso na maombolezo. Kwa maana anaendelea kusema moyoni mwake: 'Ninaketi nikiwa malkia, mimi si mjane, nami sitaona maombolezo kamwe.'^f **8** Hiyo ndiyo sababu mipigo yake yatakuja katika siku moja, kifo na kuomboleza na njaa kali, naye atateketezwa kabisa kwa moto,^g kwa sababu Yehova* Mungu, aliyemhukumu, ni mwenye nguvu.^h

9 "Na wafalme wa dunia waliofanya uasherati* naye na kuishi naye katika anasa isiyo na aibu watalia na kujipigapiga kwa huzuni kwa sababu yake watakapoona moshi unaotokana na kuteke-tea kwake. **10** Watasimama mbali kwa sababu ya kuogopa kuteseka kwake na kusema: 'Ole, ole, wewe jiji kubwa,ⁱ Babiloni wewe jiji lenye nguvu, kwa sababu hukumu yako imefika katika saa moja!'

11 "Pia, wafanyabiashara wa dunia wanalia na kuomboleza kwa sababu yake, kwa kuwa hakuna yeyote wa kununua tena bidhaa zao zilizojaa, **12** mizigo iliyojaa ya dhahabu, fedha, mawe ya thamani, lulu, kitani bora, vitambaa vya zambarau, hariri, na vitambaa vyekundu; na kila kitu

SURA YA 18

a Ufu 16:19

b Yer 50:29
2Th 1:6c Zb 137:8
Yer 50:15

d Zb 75:8

e Ufu 16:19

f Isa 47:7-9

g Law 21:9

h Yer 50:34

i Da 4:30

Safu ya 2

a Ufu 17:4

kilichotengenezwa kwa mbao zenye manukato; na kila aina ya kitu kilichotengenezwa kwa pembe za tembo, na kwa mbao za thamani, shaba, chuma, na marumaru; **13** pia mdalasini, viungo vya Kihindi, uvumba, mafuta yenye marashi, ubani, divai, mafuta ya zeituni, unga laini, ngano, ng'ombe, kondoo, farasi, magari, watumwa, na uhai wa binadamu.* **14** Ndiyo, tunda zuri ulilotamani* limekuacha, na vitu vyote vitamu na vitu vyenye fahari vimetoweka kutoka kwako, navyo havitapatikana tena kamwe.

15 "Wafanyabiashara waliouza vitu hivyo, waliopata utajiri kutokana naye, watasimama mbali kwa sababu ya kuogopa kuteseka kwake nao watalia na kuomboleza, **16** wakisema: 'Ole, ole, lile jiji kubwa lililovaa kitani bora, zambarau, na kitambaa chekundu, na lililopambwa sana kwa mapambo ya dhahabu, mawe ya thamani, na lulu,^a **17** kwa sababu katika saa moja mali nyingi hivyo zimeharibiwa!'

"Na kila kapteni wa meli na kila mtu anayesafiri baharini na mabaharia na wale wote ambao hupata riziki baharini walisimama mbali **18** na kusema kwa sauti kubwa huku wakitazama moshi uliotokana na kuteketezwa kwake: 'Ni jiji gani lililo kama lile jiji kubwa?' **19** Wakatupa mavumbi juu ya vichwa vyao na kupaza kilio, wakilia na kuomboleza, wakisema: 'Ole, ole, lile jiji kubwa, ambalo wale wote waliokuwa na meli baharini waliokuwa matajiri kutokana na

18:5 *Au "uhalifu wake." 18:8 *Angalia Nyongeza A5. 18:9 *Angalia Kamusi, uku. 2012.

18:13 *Au "nafsi za binadamu." 18:14 *Au "ambalo nafsi yako ililitamani."

utajiri wake, kwa sababu katika saa moja ameharibiwa!^a

20 “Furahini kwa sababu yake, enyi mbingu,^b pia ninyi watakatifu^c na mitume na manabii, kwa sababu Mungu ametangaza hukumu juu yake kwa ajili yenu!”^d

21 Na malaika mwenye nguvu akainua jiwe lililo kama jiwe kubwa la kusagia na kulitupa baharini, akisema: “Hivi ndivyo Babiloni lile jiji kubwa litakavyotupwa chini kwa kasi sana, naye hatapatikana tena.”^e **22** Na sauti ya waimbaji ambao hufuatanisha sauti zao kwa kinubi, ya wanamuziki, ya wapiga-filimbi, na ya wapiga-tarumbeta haitasikiwa tena ndani yako. Na hakuna fundi anayefanya kazi yoyote atakayepatikana tena ndani yako, na hakuna sauti ya jiwe la kusagia itakayosikiwa tena ndani yako. **23** Hakuna nuru ya taa itakayoangaza tena ndani yako, na hakuna sauti ya bwana harusi na bibi harusi itakayosikiwa tena ndani yako; kwa kuwa wafanyabiashara wako walikuwa watu wenye vyeo vya juu duniani, kwa maana mataifa yote yalipotoshwa kwa mazoea yako ya kuwasiliana na roho.^f **24** Ndiyo, ndani yake ilipatikana damu ya manabii na ya watakatifu^g na ya wale wote ambao wameuawa duniani.”^h

19 Baada ya hayo nikasikia kitu kama sauti kubwa ya umati mkubwa mbinguni. Wakasema: “Msifuni Yah!”ⁱ Wokovu na utukufu na nguvu ni za Mungu

19:1, 3, 4, 6 *Au “Haleluya!” “Yah” ni ufupisho wa jina Yehova.

SURA YA 18

a Isa 47:11

b Yer 51:48

c Ufu 14:12

d Kum 32:43
Ro 12:19
Ufu 6:9,10
Ufu 19:1, 2

e Yer 51:63, 64

f Isa 47:9
Gal 5:19, 20g Ufu 6:9,10
Ufu 16:5, 6h Mwa 9:6
Yer 51:49

SURA YA 19

i Zb 150:6

Safu ya 2

a Kum 32:4
Zb 19:9
Ufu 15:3b Kum 32:43
2Fa 9:7
Zb 79:10
Ufu 18:20, 24

c Zb 117:1

d Isa 34:10

e Ufu 4:4

f Ufu 4:6

g Zb 106:48

h Zb 134:1
Zb 135:1

i Zb 115:13

j Zb 113:1

k Kut 6:3

l Zb 97:1
Isa 52:7
Ufu 11:15m Isa 61:10
Efe 5:25-27
Ufu 14:4

wetu, **2** kwa sababu hukumu zake ni za kweli na za uadilifu.^a Kwa maana ametekeleza hukumu juu ya yule kababa mkubwa aliyeipotoshia dunia kwa uasherati* wake, naye amelipiza kisasi damu ya watumwa wake iliyo mkononi mwake.”^{#b} **3** Na papo hapo, wakasema kwa mara ya pili: “Msifuni Yah!”^{*c} Na moshi kutoka wakasema[#] unaendelea kupanda milele na milele.”^d

4 Na wale wazee 24^e na wale viumbe hai wanne^f wakaanguka chini na kumwabudu Mungu anayeketi kwenye kiti cha ufalme na kusema: “Amina! Msifuni Yah!”^{*g}

5 Pia, sauti ikatoka katika kile kiti cha ufalme na kusema: “Endeleeni kumsifu Mungu wetu, enyi nyote watumwa wake^h mnaomwogopa, wadogo kwa wakubwa.”ⁱ

6 Nami nikasikia kitu kama sauti ya umati mkubwa na kama sauti ya maji mengi na kama sauti ya ngurumo nzi-to. Wakasema: “Msifuni Yah,^{*j} kwa sababu Yehova[#] Mungu wetu, Mweza-Yote,^k ameanza kutawala akiwa mfalme!” **7** Acheni tufurahi na tuwe na shangwe nyingi na tumpe utukufu, kwa sababu ndoa ya Mwanakondoo imefika na mke wake amejitayarisha. **8** Ndiyo, ameruhusiwa kuvaa kitani bora, changavu, safi—kwa maana hicho kitani bora kinamaanisha matendo ya uadilifu ya watakatifu.”^m

9 Naye ananiambia, “Andika: Wenye furaha ni wale wa-

19:2 *Neno la Kigiriki *pornei*’a. Angalia Kamusi, uku. 2012. [#]Tnn., “kutoka mkononi mwake.” **19:3** *Yaani, “kutoka kwa Babiloni.” **19:6** #Angalia Nyo-geza A5.

lialikwa kwenye mlo wa jioni wa ndoa ya Mwanakondoo.”^a Pia, ananiambia: “Hayo ndiyo maneno ya kweli ya Mungu.” **10** Ndipo nikaanguka chini mbele ya miguu yake ili kuwabudu. Lakini ananiambia: “Uwe mwangalifu! Usifanye hivyo!”^b Mimi ni mtumwa mwenzako tu na wa ndugu zako walio na kazi ya kutoa ushahidi kumhusu Yesu.^c Mwabudu Mungu!^d Kwa maana kutoa ushahidi kumhusu Yesu ndilo kusudi la unabii.”^e

11 Nami nikaona mbingu imefunguliwa, na tazama! farasi mweupe.^f Na yule aliyeketi juu yake anaitwa Mwaminifu^g na wa Kweli,^h naye anakumu na kupigana vita kwa uadilifu.ⁱ **12** Macho yake ni mwali wa moto,^j na juu ya kichwa chake kuna mataji mengi.* Ana jina lililoandikwa ambalo hakuna yeyote anayelijua isipokuwa yeye mwenyewe, **13** naye amevaa vazi la nje lililo na damu,* na jina analoitwa ni Neno^k la Mungu. **14** Pia, majeshi ya mbinguni yalikuwa yakimfuata juu ya farasi weupe, nayo yalikuwa yamevaa kitani bora cheupe, safi. **15** Na kinywani mwake upanga mrefu mkali unachomoza,^l upanga ambao atatumia kuyapiga mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma.^m Isitoshe, anakanyaga shinikizo la divai ya hasira ya ghadhabu ya Mungu Mweza-Yote.ⁿ **16** Na kwenye vazi lake la nje, ndiyo, kwenye paja lake, ana jina lililoandikwa, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.^o

19:12 *Au “tepe nyingi za kichwani za kifalme.” **19:13** *Au labda, “lililonyuni-ziwa damu.”

SURA YA 19

- a Mt 22:2
Mt 25:10
b Mdo 10:25, 26
Ufu 22:8, 9
c Mt 28:19, 20
Mdo 1:8
d Mt 4:10
Yoh 4:23
e Lu 24:27
Mdo 10:43
1Pe 1:10, 11
f Ufu 6:2
g Ufu 1:5
h Yoh 1:14
Ufu 3:14
i Isa 11:4, 5
Ebr 1:8, 9
j Ufu 1:13, 14
k Yoh 1:1
l 2Th 2:8
Ufu 1:13, 16
m Zb 2:9
Ufu 2:26, 27
n Yoe 3:13
Ufu 14:19, 20
o Mt 28:18
Flp 2:9-11
1Ti 6:15
Ufu 17:14

Safu ya 2

- a Eze 39:4, 17
b Eze 39:18
c Eze 39:20
d Ufu 16:14, 16
e Ufu 16:13
f Ufu 13:16, 17
g Ufu 13:15
h Mt 10:28
2Pe 2:6
Yud 7
Ufu 20:14
i Ufu 2:16
Ufu 6:2
j Eze 39:4

SURA YA 20

- k Ufu 9:1
l Ufu 12:3
m Mwa 3:1
n Yoh 8:44

17 Nikaona pia malaika amesimama katika jua, naye akaita kwa sauti kubwa na kuwaambia ndege wote wanaoruka katikati ya mbingu:* “Njooni hapa, mkusanyike pamoja kwenye mlo mkubwa wa jioni wa Mungu,^a **18** ili mle nyama za wafalme na nyama za viongozi wa kijeshi na nyama za watu wenye nguvu^b na nyama za farasi na za wale wanaoketi juu yao,^c na nyama za wote, za watu huru na vile-vile za watumwa na za wado-gu kwa wakubwa.”

19 Nami nikamwona yule mnyama wa mwituni na wafalme wa dunia na majeshi yao wamekusanyika pamoja ili kupigana vita na yule anayeketi juu ya farasi na jeshi lake.^d **20** Na yule mnyama wa mwituni akakamatwa, na yule nabii^e wa uwongo pamoja naye, aliyefanya mbele yake ishara alizotumia kuwapotosha wale waliopokea alama ya yule mnyama wa mwituni^f na wale wanaoiabudu sanamu yake.^g Wakiwa bado hai, wote wawili walitupwa ndani ya ziwa la moto linalowaka kwa kiberiti.^h **21** Lakini wale wengine wakauawa kwa ule upanga mrefu unachomoza kinywani mwa yule anayeketi juu ya farasi.ⁱ Na ndege wote wakashi-ba kutokana na nyama zao.^j

20 Nami nikamwona malai-ka akishuka kutoka mbinguni akiwa na ufunguo wa shimo refu lisilo na mwisho*^k na mnyororo mkubwa mkononi mwake. **2** Akamakamata yule joka,^l yule nyoka wa zamani,^m ambaye ni Ibilisiⁿ

19:17 *Au “katikati ya anga; juu.” **20:1** *Au “abiso.” Angalia Kamusi, uku. 2012.

na Shetani,^a na kumfunga kwa miaka 1,000. **3** Naye akamtupa katika shimo refu lisilo na mwisho^{*b} akalifunga na kulitia muhuri juu yake, ili asipotoshe mataifa tena mpaka ile miaka 1,000 itakapokwish. Baada ya hapo atafunguliwa kwa muda mfupi.^c

4 Nami nikaona viti vya ufalme, na wale walioketi kwenye viti hivyo wakapewa mamlaka ya kuhukumu. Ndiyo, niliona nafsi* za wale waliouawa[#] kwa sababu ya ushahidi waliotoa kumhusu Yesu na kwa sababu ya kusema kumhusu Mungu, na wale ambao hawakumwabudu yule mnyama wa mwituni au sanamu yake na ambao hawakupokea ile alama kwenye paji la uso wao na kwenye mkono wao.^d Nao wakawa hai na kutawala wakiwa wafalme pamoja na Kristo^e kwa miaka 1,000.

5 (Wale wafu^f wengine hawakuwa hai mpaka ile miaka 1,000 ilipokwisha.) Huo ndio ufufuo wa kwanza.^g **6** Mwenye furaha na mtakatifu ni yeyote aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza;^h kifo cha piliⁱ hakina mamlaka juu ya hao,^j bali watakuwa makuhani^k wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala wakiwa wafalme pamoja naye ile miaka 1,000.^l

7 Sasa mara tu ile miaka 1,000 itakapokwisha, Shetani atafunguliwa kutoka katika gereza lake, **8** naye ataenda kuyapotosha yale mataifa yaliyo katika pembe nne

20:3 *Au "abiso." Angalia Kamusi, uku. 2012. 20:4 *Angalia Kamusi, uku. 2012 na Maelezo ya chini ya Ufu 6:9. #Tnn., waliouawa kwa shoka."

SURA YA 20

a Zek 3:1
Ufu 12:9

b Ufu 9:11

c Ufu 20:7

d Ufu 13:15-17

e Mt 19:28
Lu 22:28-30
2Ti 2:12
Ufu 1:6

f Mdo 24:15

g 1Ko 15:23, 52
Flp 3:10, 11
1Th 4:16

h Ufu 14:13

i Ufu 2:11
Ufu 20:14

j 1Ko 15:54

k 1Pe 2:9

l Ufu 1:6
Ufu 5:9, 10

Safu ya 2

a 2Fa 1:10

b Ufu 13:1

c Ufu 19:20

d Ufu 4:2, 3

e 2Pe 3:7

f Kut 32:33
Zb 69:28
Da 12:1

g Yoh 5:28, 29

h Mdo 10:42

i Isa 25:8
1Ko 15:26

j Ufu 2:11
Ufu 20:6

k Mt 5:22
Mt 18:9
Ufu 21:8

za dunia, Gogu na Magogu, ili kuwakusanya pamoja kwa ajili ya vita. Idadi yao ni kama mchanga wa bahari. **9** Nao wakaenda katika dunia yote na kuizunguka kambi ya watakatifu na lile jiji linalopendwa. Lakini moto ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza.^a **10** Na Ibilisi aliyekuwa akiwapotosha alitupwa ndani ya lile ziwa la moto na kiberiti, ambamo wote wawili, yule mnyama wa mwituni^b na yule nabii wa uwongo, tayari walikuwa;^c nao watateswa* mchana na usiku milele na milele.

11 Nami nikaona kiti cha ufalme kikubwa cheupe na Yule aliyeketi juu yake.^d Dunia na mbingu zikatoweka kutoka mbele zake,^e na hazikupatikana tena. **12** Nami nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wakiwa wamesimama mbele ya kile kiti cha ufalme, na vitabu vya kukunjwa vikafunguliwa. Lakini kitabu kingine cha kukunjwa kikafunguliwa; hicho ni kitabu cha uzima.^f Wafu wakahukumiwa kutokana na yale mambo yaliyoandikwa katika vile vitabu kulingana na matendo yao.^g **13** Na bahari ikawatoa wafu waliokuwa ndani yake, na kifo na Kaburi* vikawatoa wafu waliokuwa ndani yake, nao wakahukumiwa kila mmoja kulingana na matendo yake.^h **14** Na kifo na Kaburi* vikatupwa ndani ya lile ziwa la moto.ⁱ Hilo linamaanisha kifo cha pili,^j lile ziwa la moto.^k **15** Zaidi ya hayo, yeyote ambaye hakupatikana ameandikwa katika kile kita-

20:10 *Au "watazuliwa; watafungwa gerezani." 20:13, 14 *Au "Hadesi." Angalia Kamusi, uku. 2012.

bu cha uzima^a alitupwa ndani ya lile ziwa la moto.^b

21 Nami nikaona mbingu mpya na dunia mpya;^c kwa maana mbingu ya kwanza na dunia ya kwanza zilikuwa zimepitilia mbali,^d na bahari^e haipo tena. **2** Pia, nikaona lile jiji takatifu, Yerusalemu Jipya, likishuka kutoka mbinguni kwa Mungu^f likiwa limetayarishwa kama bibi harusi aliyepambwa kwa ajili ya mume wake.^g **3** Ndipo nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha ufalme iki-sema: "Tazama! Hema la Mungu liko pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.^h **4** Naye atafuta kila chozi kutoka katika macho yao,ⁱ na kifo hakitakuwapo tena,^j wala maombolezo wala kilio wala maumivu hayatakuwapo tena.^k Mambo ya zamani yamepitilia mbali."

5 Na Yule aliyeketi kwenye kiti cha ufalme^l akasema: "Tazama! Ninafanya vitu vyote kuwa vipya."^m Pia anasema: "Andika, kwa maana maneno haya ni ya uaminifu* na ya kweli." **6** Naye akaniambia: "Yametimia! Mimi ndiye Alfa na Omega,* mwanzo na mwisho.ⁿ Yeyote aliye na kiu nita-mpa maji bure^o kutoka kwenye chemchemi^a ya maji ya uzima.^o **7** Yeyote anayeshinda atarithi vitu hivi, nami nitakuwa Mungu wake naye atakuwa mwanangu. **8** Lakini kuhusu waoga na wale wasio

21:5 *Au "kutegemeka." 21:6 *Au "herufi A na Z." Alfa ni herufi ya kwanza na Omega ni herufi ya mwisho katika alfa-beti ya Kigiriki. ^aAu "bila gharama." ^aAu "mabubujiko."

SURA YA 20

a Ufu 17:8

b Met 10:7

SURA YA 21

c Isa 65:17

Isa 66:22

2Pe 3:13

d 2Pe 3:10

Ufu 20:11

e Isa 57:20

f Ufu 3:12

g Ufu 19:7

h Eze 37:27

i Ufu 7:17

j Isa 25:8

1Ko 15:26

k Isa 35:10

Isa 65:19

l Ufu 4:2, 3

m 2Pe 3:13

n Ufu 1:8

Ufu 22:13

o Zb 36:9

Isa 55:1

Ufu 7:17

Ufu 22:1

Safu ya 2

a 1Yo 5:10

b 1Yo 3:15

c Efe 5:5

d Yoh 8:44

e Ufu 19:20

f Met 10:7

Ebr 10:26, 27

Ufu 2:11

Ufu 20:6

g Ufu 15:1

h Ufu 19:7

i Ebr 12:22

Ufu 3:12

Ufu 21:2

j Isa 60:1, 2

k Kut 24:9, 10

l Ufu 22:14

m Mt 10:2-4

Lu 6:13-16

Mdo 1:13

na imani^a na wale wenye kuchukiza katika uchafu wao na wauaji^b na waasherati*^c na wale wanaozoea kuwasiliana na roho na wanaoabudu sanamu na waongo wote,^d fungu yao litakuwa ndani ya lile ziwa linalowaka moto na kiberiti.^e Hili linamaanisha kifo cha pili."^f

9 Mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na mabakuli saba yaliyojaa mapigo saba ya mwisho^g akaja na kuniambia: "Njoo, nami nitakuonyesha bibi harusi, mke wa Mwanakondoo."^h **10** Basi akani-chukua katika nguvu za roho akanipeleka kwenye mlima mkubwa na mrefu sana, naye akanionyesha lile jiji takatifu Yerusalemu likishuka kutoka mbinguni kwa Munguⁱ **11** na likiwa na utukufu wa Mungu.^j Mwangaza wake ulikuwa kama jiwe la thamani zaidi, kama jiwe la yaspi lenye kung'aa kwa uangavu kama fuwele.^k **12** Lilikuwa na ukuta mkubwa na mrefu sana nalo lilikuwa na malango 12, na malaika 12 kwenye malango hayo, na majina ya makabila 12 ya wana wa Israeli yalikuwa yameandikwa kwenye malango hayo. **13** Upande wa mashariki kulikuwa na malango matatu, upande wa kaskazini malango matatu, upande wa kusini malango matatu, na upande wa magharibi malango matatu.^l **14** Ukuta wa lile jiji pia ulikuwa na mawe ya msingi 12, na juu ya mawe hayo kulikuwa na majina 12 ya mitume 12^m wa Mwanakondoo.

21:8 *Angalia Kamusi, uku. 2012, "Uasherati."

15 Basi yule aliyekuwa aki-zungumza nami alikuwa ameshika utete wa kupimia wa dhahabu ili alipime lile jiji na malango yake na ukuta wake.^a

16 Na lile jiji lilikuwa mra-ba, na urefu wake ni mkubwa kama upana wake. Naye akalipima jiji kwa utete, stadia 12,000;* urefu wake na upana wake na kimo chake ni sawa.

17 Pia, akapima ukuta wake, mikono 144,* kulingana na kipimo cha mwanadamu, na wakati huohuo kipimo cha malaika.

18 Basi ule ukuta ulitengenezwa kwa yaspi,^b na jiji lilikuwa dhahabu safi kama kioo safi.

19 Misingi ya ukuta wa jiji ilikuwa imepambwa kwa kila namna ya jiwe la thamani: msingi wa kwanza ulikuwa yaspi, wa pili yakuti, wa tatu kalkedoni, wa nne zumaridi,

20 wa tano sardoniksi, wa sita sardio, wa saba krisolito, wa nane beroli, wa tisa topazi, wa kumi krisopraso, wa kumi na moja hayasinthi, wa kumi na mbili amethisto.

21 Pia, yale malango 12 yalikuwa lulu 12; kila lango lilitengenezwa kwa lulu moja. Na barabara kuu ya jiji ilikuwa dhahabu safi, kama kioo kiangavu.

22 Sikuaona hekalu ndani yake, kwa maana Yehova* Mungu Mweza-Yote^c ndiye hekalu lake, na pia Mwanakondoo.

23 Na lile jiji halihitaji jua wala mwezi kuliangazia, kwa maana utukufu wa Mungu uli-liangazia,^d na taa yake ilikuwa yule Mwanakondoo.^e

24 Na

21:16 *Karibu kilomita 2,220 (maili 1,379). Stadiumu moja ilikuwa sawa na mita 185 (futi 606.95). Angalia Nyongeza B14. 21:17 *Karibu mita 64 (futi 210). Angalia Nyongeza B14. 21:22; 22:5 *Angalia Nyongeza A5.

SURA YA 21

a Eze 40:3, 5

b Ufu 4:3
Ufu 21:10, 11

c Kut 6:3

d Isa 60:19, 20
Ufu 22:5

e Yoh 1:9
Mdo 26:13, 15
Ebr 1:3

Safu ya 2

a Isa 60:3

b Isa 60:11, 20

c Isa 60:5

d Zb 5:6
Isa 52:1
1Ko 6:9, 10
Gal 5:19-21
Ufu 21:8

e Da 12:1
Flp 4:3
Ufu 13:8

SURA YA 22

f Eze 47:1

g Yoh 1:29

h Eze 47:12

i Ufu 3:21

j Mt 5:8

k Ufu 14:1

l Ufu 21:25

m Isa 60:19, 20
1Yo 1:5

n Da 7:18
Ufu 3:21

o Tit 1:2

mataifa yatatembea kwa nuru yake,^a na wafalme wa dunia wataleta utukufu wao ndani yake.

25 Malango yake hayatafungwa kamwe mchana, kwa maana hakutakuwa na usiku humo.^b

26 Nao wataleta utukufu na heshima ya mataifa ndani yake.^c

27 Lakini chochote kilicho najisi na yoyote anayetenda mambo yanayochukiza na ya udanganyifu hataingia kamwe humo;^d watakaoingia ni wale tu walioandikwa katika kile kitabu cha kukunjwa cha uzima cha Mwanakondoo.^e

22 Naye akanionyesha mto wa maji ya uzima,^f mwangavu kama fuwele, ukitiririka kutoka katika kiti cha ufalme cha Mungu na cha Mwanakondoo^g

2 kiteremka kati-
kati ya barabara yake kuu. Pande zote mbili za ule mto zilikuwa na miti ya uzima iliyo-
zaa mazao 12 ya matunda, iki-
zaa matunda yake kila mwezi.

Na majani ya ile miti yalikuwa ya kuponya mataifa.^h

3 Na hakutakuwa tena na laana yoyote. Bali kiti cha ufalme cha Mungu na cha Mwanakondooⁱ kitakuwa kati-
ka jiji hilo, na watumwa wake wataamtolea utumishi mtaka-
tifu; 4 nao watauona uso
wake,^j na jina lake litakuwa
kwenye mapaji ya nyuso zao.^k

5 Pia, hakutakuwa na usiku tena,^l na hawahitaji nuru ya taa au ya jua, kwa maana Ye-
hova* Mungu ataangaza nuru
yake juu yao,^m nao watatawala
wakiwa wafalme milele na mi-
lele.ⁿ

6 Akaniambia: "Maneno haya ni ya uaminifu* na ya kweli;^o

22:6 *Au "kutegemeka."

ndiyo, Yehova,* Mungu aliyewaongoza manabii,^a alimtumama laika wake ili kuwaonyesha watumwa wake mambo ambayo lazima yatendeke upesi. **7** Tazama! Ninakuja upesi.^b Mwenye furaha ni yeyote anayeshika maneno ya unabii wa kitabu hiki cha kukunjwa.”^c

8 Basi mimi, Yohana, ndiye niliyekuwa nikisikia na kuona mambo haya. Niliposikia na kuyaona, nikaanguka chini kuabudu miguuni pa yule malaika aliyekuwa akinionyesha mambo haya. **9** Lakini yeye akaniambia: “Uwe mwangalifu! Usifanye hivyo! Mimi ni mtumwa mwenzako tu na wa ndugu zako manabii na wa wale wanaoshika maneno ya kitabu hiki cha kukunjwa. Mwabudu Mungu.”^d

10 Pia akaniambia: “Usiyatie muhuri maneno ya unabii wa kitabu hiki cha kukunjwa, kwa maana wakati uliowekwa uko karibu. **11** Yule anayetenda ukosefu wa uadilifu na aendelee kutenda ukosefu wa uadilifu, na mwenye uchafu aendelee katika uchafu wake; lakini mwadilifu na aendelee kufanya uadilifu, na mtakatifu aendelee katika utakatifu.

12 “Tazama! Ninakuja upesi, nikiwa na thawabu ninayotoa, ili kumlipa kila mmoja kulingana na matendo yake.”^e

13 Mimi ndiye Alfa na Omega,^{*f} wa kwanza na wa mwisho, mwanzo na mwisho.

14 Wenye furaha ni wale wanaofua kanzu zao,^g ili wawe na mamlaka ya kwenda kwe-

22:6 *Angalia Nyongeza A5. 22:13 *Au “herufi A na Z.” Alfa ni herufi ya kwanza na Omega ni herufi ya mwisho katika alfabeti ya Kigiriki.

SURA YA 22

a 2Ti 3:16

b Ufu 16:15
Ufu 22:20c Yoh 13:17
Ufu 1:3d Mt 4:10
Mdo 10:25, 26
Ufu 19:10e Zb 62:12
Isa 40:10
Ro 2:6f Isa 44:6
Isa 48:12
Ufu 1:8
Ufu 21:6

g 1Yo 1:7

Safu ya 2

a Ufu 2:7

b Ufu 21:10, 12

c Gal 5:19-21
Efe 5:5
Ufu 21:8d Isa 11:1, 10
Isa 53:2
Yer 23:5
Yer 33:15
Ufu 5:5e Hes 24:17
Ufu 2:28

f Ufu 21:9

g Yoh 4:14

h Isa 55:1
Yoh 7:37
Ufu 7:17
Ufu 21:6i Kum 4:2
Kum 12:32
Gal 1:8
1Yo 4:3
2Yo 9

j Ufu 15:1

k Ufu 2:7

l Ufu 21:2

m Ufu 3:11
Ufu 22:7

nye miti ya uzima^a na waweze kuingia katika jiji kupitia malango yake.^b **15** Nje kuna mbwa* na wale walio na mazoea ya kuwasiliana na roho, waasherati,[#] wauaji, waabudu-sanamu, na kila mtu anayependa uwongo na aliye na mazoea ya kusema uwongo.^c

16 “Mimi, Yesu, nilimtumama laika wangu kuwatolea ninyi ushahidi kuhusu mambo haya kwa ajili ya makutaniko. Mimi ndiye mzizi na uzao wa Daudi^d na nyota nyangavu ya asubuhi.”^e

17 Na roho na bibi harusif^f huendelea kusema, “Njoo!” na yeyote anayesikia na aseme, “Njoo!” na yeyote aliye na kiu aje;^g yeyote anayetaka achukue maji ya uzima bure.^h

18 “Ninamtotea ushahidi kila mtu anayesikia maneno ya unabii wa kitabu hiki cha kukunjwa: Yeyote akiongeza kwenye mambo haya,ⁱ Mungu atamwongezea mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki;^j **19** na yeyote akiondoa lolote kutoka katika maneno ya kitabu cha unabii huu, Mungu ataondoa fungu lake kutoka katika ile miti ya uzima^k na kutoka katika lile jiji takatifu,^l mambo yaliyoandikwa katika kitabu hiki cha kukunjwa.

20 “Yule anayetoa ushahidi kuhusu mambo haya anasema, ‘Ndiyo, mimi ninakuja upesi.’”^m

“Amina! Njoo, Bwana Yesu.”
21 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana Yesu na ziwe pamoja na watakatifu.

22:15 *Yaani, wale ambao matendo yao yanamchukiza Mungu. #Angalia Kamusi, uku. 2012, “Uasherati.”

Orodha ya Vitabu vya Biblia

Vitabu vya Maandiko ya Kiebrania Kabla ya Wakati wa Kawaida (wa Ukristo)

Jina la Kitabu	Mwandikaji	Mahali Kilipoandikiwa	Uandikaji Ulikamilishwa (K.W.K.)	Muda Unaohusika (K.W.K.)
Mwanzo	Musa	Nyikani	1513	"Hapo mwanzo" mpaka 1657
Kutoka	Musa	Nyikani	1512	1657-1512
Mambo ya Walawi	Musa	Nyikani	1512	Mwezi 1 (1512)
Hesabu	Musa	Nyikani na Nchi Tambarare za Moabu	1473	1512-1473
Kumbukumbu la Torati	Musa	Nchi Tambarare za Moabu	1473	Miezi 2 (1473)
Yoshua	Yoshua	Kanaani	m. 1450	1473-m. 1450
Waamuzi	Samweli	Israeli	m. 1100	m. 1450-m. 1120
Ruthu	Samweli	Israeli	m. 1090	Miaka 11 ya utawala wa Waamuzi
1 Samweli	Samweli; Gadi; Nathani	Israeli	m. 1078	m. 1180-1078
2 Samweli	Gadi; Nathani	Israeli	m. 1040	1077-m. 1040
1 Wafalme	Yeremia	Yuda na Misri	Kitabu 1	m. 1040-580
2 Wafalme	Yeremia		580	
1 Mambo ya Nyakati	Ezra	Yerusalemu (?)	Kitabu 1	[Baada ya 1 Mambo ya Nyakati 9:44: m. 1077-537
2 Mambo ya Nyakati	Ezra	Yerusalemu (?)	m. 460	
Ezra	Ezra	Yerusalemu	m. 460	537-m. 467
Nehemia	Nehemia	Yerusalemu	b. 443	456-b. 443
Esta	Mordekai	Shushani, Elamu	m. 475	493-m. 475
Ayubu	Musa	Nyikani	m. 1473	Zaidi ya miaka 140 kati ya 1657 na 1473
Zaburi	Daudi na wengine		m. 460	
Methali	Sulemani; Aguri; Lemueli	Yerusalemu	m. 717	
Mhubiri	Sulemani	Yerusalemu	k. 1000	
Wimbo wa Sulemani	Sulemani	Yerusalemu	m. 1020	
Isaya	Isaya	Yerusalemu	b. 732	m. 778-b. 732
Yeremia	Yeremia	Yuda; Misri	580	647-580
Maombolezo	Yeremia	Karibu na Yerusalemu	607	
Ezekieli	Ezekieli	Babiloni	m. 591	613-m. 591
Danieli	Danieli	Babiloni	m. 536	618-m. 536
Hosea	Hosea	Samaria (Wilaya)	b. 745	k. 804-b. 745
Yoeli	Yoeli	Yuda	m. 820 (?)	
Amosi	Amosi	Yuda	m. 804	
Obadia	Obadia		m. 607	
Yona	Yona		m. 844	
Mika	Mika	Yuda	k. 717	m. 777-717
Nahumu	Nahumu	Yuda	k. 632	
Habakuki	Habakuki	Yuda	m. 628 (?)	
Sefania	Sefania	Yuda	k. 648	
Hagai	Hagai	Yerusalemu	520	Siku 112 (520)
Zekaria	Zekaria	Yerusalemu	518	520-518
Malaki	Malaki	Yerusalemu	b. 443	

Orodha ya Vitabu vya Biblia

Vitabu vya Maandiko ya Kigiriki Vilivyoandikwa Katika Wakati wa Kawaida (wa Ukristo)

Jina la Kitabu	Mwandikaji	Mahali Kilipoandikiwa	Uandikaji Ulikamilishwa (W.K.)	Muda Unaohusika
Mathayo	Mathayo	Israeli	m. 41	2 K.W.K.–33 W.K.
Marko	Marko	Roma	m. 60-65	29-33 W.K.
Luka	Luka	Kaisaria	m. 56-58	3 K.W.K.–33 W.K.
Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	Baada ya utangulizi, 29-33 W.K.
Matendo	Luka	Roma	m. 61	33–m. 61 W.K.
Waroma	Paulo	Korintho	m. 56	
1 Wakorintho	Paulo	Efeso	m. 55	
2 Wakorintho	Paulo	Makedonia m. 55		
Wagalatia	Paulo	Korintho au Antiokia ya Siria	m. 50-52	
Waefeso	Paulo	Roma	m. 60-61	
Wafilipi	Paulo	Roma	m. 60-61	
Wakolosai	Paulo	Roma	m. 60-61	
1 Wathesalonike	Paulo	Korintho	m. 50	
2 Wathesalonike	Paulo	Korintho	m. 51	
1 Timotheo	Paulo	Makedonia	m. 61-64	
2 Timotheo	Paulo	Roma	m. 65	
Tito	Paulo	Makedonia (?)	m. 61-64	
Filemoni	Paulo	Roma	m. 60-61	
Waebrania	Paulo	Roma	m. 61	
Yakobo	Yakobo (ndugu ya Yesu)	Yerusalemu	k. 62	
1 Petro	Petro	Babiloni	m. 62-64	
2 Petro	Petro	Babiloni (?)	m. 64	
1 Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	
2 Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	
3 Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	
Yuda	Yuda (ndugu ya Yesu)	Israeli (?)	m. 65	
Ufunuo	Mtume Yohana	Patmosi	m. 96	

[Majina ya waandikaji wa vitabu fulani na ya mahali vilipoandikiwa hayajulikani kwa uhakika. Tarehe nyingi zimekadiriwa tu, herufi b. inamaanisha "baada ya," k. inamaanisha "kabla ya" na m. inamaanisha "mnamo" au "karibu."]

Ufupisho Uliotumiwa Katika Maelezo ya Chini

Tnn., Tafsiri ya neno kwa neno

Fahirisi ya Maneno ya Biblia

Ili kupata ufupisho wa majina ya vitabu vya Biblia angalia ukurasa wa 40.

A

ABBA, Ro 8:15 tunapaza sauti: *Abba*, Baba!
ABELI, Mwa 4:8 Kaini akamshambulia *Abeli*
Mt 23:35 kuanzia damu ya *Abeli* mwadilifu
ABIGAILI, 1Sa 25:3 *Abigaili* mwenye busara na mrembo
ABRAHAMU, Mwa 21:12 *Abrahamu*, msikilize Sara
2Ny 20:7 rafiki yako *Abrahamu*
Mt 22:32 Mungu wa *Abrahamu* na Isaka
Ro 4:3 *Abrahamu* mwenye imani, ahesabiwa
ABUDU, Kut 34:14 watu *waniabudu mimi peke yangu*
ACHA, Isa 1:28 *wanaowacha* Yehova watafikia mwisho
Mt 19:29 ambaye *ameacha* nyumba au
ACHILIWA, Met 29:15 mtoto *aliyeachiliwa* humwaibisha
ADABU, Ro 13:13 tujendeshe kwa *adabu*
1Ko 14:40 yote yatendeke kwa *adabu*
ADAMU, Mwa 5:5 *Adamu* alishi miaka 930, kisha akafa
1Ko 15:22 katika *Adamu* wote wanakufa
1Ko 15:45 *Adamu* wa mwisho akawa
1Ti 2:14 *Adamu* hakudanganywa, bali mwanamke
ADUI, Mt 5:44 Endeleeni kuwepanda *adui* zenu
Mt 10:36 *adui* za mtu watakuwa watu wa
Ro 12:20 ikiwa *adui* yako ana njaa, mlishe
AGANO, Mwa 15:18 Yehova alifanya *agano* na Abram
Yer 31:31 nitafanya *agano* jipya
Lu 22:20 *agano* jipya kwa msingi wa damu yangu
Lu 22:29 ninafanya *agano* pamoja nanyi
AHADI, 1Fa 8:56 Hakuna *ahadi* yoyote iliyokosa kutimia
Zb 15:4 Havunji *ahadi* yake, hata ikimletea hasara
2Ko 1:20 *ahadi* za Mungu "ndiyo" kupitia yeye
AHIDI, Ebr 10:23 yule *aliyeahidi* ni mwaminifu
AHIRISHA, Met 13:12 Mataraji *yalioahirishwa* hufanya
AIBU, Ebr 9:6 ninaona *aibu* kuunua usi wangu
Zb 25:3 yeyote anayekutumaini *hataaibishwa*
Mk 8:38 atakayeniona *aibu* mimi na
Ro 1:16 sionei *aibu* habari njema
1Ko 4:14 si ili *niwaabishe*, bali niwaonye
Efe 5:4 mwenendo wa *aibu* wala maneno ya
2Ti 1:8 usione *aibu* kuhusu ushahidi
2Ti 2:15 mfanyakazi asiye na la kuonea *aibu*
Ebr 11:16 Mungu haoni *aibu* kuwahusu
1Pe 4:16 akiteseka akiwa Mkristo, asione *aibu*
AINA, 2Pe 3:11 mnapaswa kuwa watu wa *aina* gani
AKANI, Yos 7:1 *Akani* alichukua baadhi ya
AKILA, Mdo 18:2 akamkuta Myahudi aliyelitwa *Akila*
AKILI, Zb 8:4 Mwanadamu ni nini, unamwaka *akilini*?
Isa 65:17 mambo ya zamani hayataingia tena *akilini*?
Mt 22:37 umpedee Yehova kwa *akili* yako yote
Mdo 9:22 akithibitisha kupatana na *akili*
Ro 7:25 kwa *akili* mimi ni mtumwa wa sheria
Ro 8:6 kukaza *akili* kwenye mwili, kifo
1Ko 2:16 tunayo *akili* ya Kristo
Efe 4:23 upya katika nguvu zinazongoza *akili*
Flp 3:19 *akili* zao zinafikiria vitu vya duniani
Kol 3:2 kukaza *akili* kwenye mambo yaliojuu
ALAMA, Eze 9:4 uyatie *alama* mapaji ya nyuso za watu
2Th 3:14 mtieni *alama*, msishirikiane naye
Ufu 13:17 isipokuwa mtu aliye na ile *alama*
ALFA, Ufu 1:8 *Alfa* na Omega
ALIKWA, Mt 22:14 wengi *waalikwa*, wachache wachaguliwa
ALIYE JUU ZAIDI, Zb 83:18 Yehova, ndiye *Uliye Juu Zaidi*
Da 4:17 wajue *Aliye Juu Zaidi* ni Mtawala
AMANI, Zb 29:11 atawabariki watu wake kwa *amani*
Zb 37:11 watafurahia kwelikweli wangi wa *amani*
Zb 72:7 *amani* itakuwa nyingi mpaka mwezi haupo
Zb 119:165 wanaoipenda sheria wana *amani*
Met 17:1 afadhali kipande cha mkate penye *amani*
Isa 9:7 Kwa wingi wa *amani*, hakuna mwisho
Isa 32:18 makao ya kudumu yenye *amani*

Isa 48:18 *amani* yako ingekuwa kama mto
Isa 54:13 *amani* ya wana wako itakuwa nyingi
Isa 57:21 Hakuna *amani* kwa waovu
Isa 60:17 Nitaweka *amani* kuwa wangaalizi wako
Yer 6:14 Kuna *amani!* Wakati hakuna *amani*
Mt 5:9 Wenye furaha ni wanaofanya *amani*
Mt 5:24 Kwanza fanya *amani* na ndugu yako
Mk 9:50 mdumishe *amani* kati yenu
Yoh 14:27 Ninawaachia *amani*; ninawapa *amani*
Mdo 9:31 kutaniko likaingia kipindi cha *amani*
Ro 5:1 tufurahie *amani* pamoja na Mungu
Ro 8:6 kukaza *akili* kwenye roho, *amani*
Ro 12:18 fanyeni *amani* na watu wote
Flp 4:7 *amani* ya Mungu itailinda mioyo yenu
1Th 5:3 *amani* na usalama! uharifibu wa ghafila
1Pe 3:11 atafute *amani* na kufuatilia
Ufu 6:4 akapewa ruhusa kuondoa *amani* duniani
AMINA, Kum 27:15 wote wataesema, *Amina!*
1Ko 14:16 *Amina* unapotoa shukrani
2Ko 1:20 kupitia yeye *Amina* husema
AMINI, Yoh 20:29 Wenye furaha wanaamini bila kuona
2Th 2:12 hawakuamini kweli, bali
AMRI, Mt 22:40 na Manabii hutegeema *amri* hizo mbili
Mk 12:28 Ni *amri* gani iliyo ya kwanza?
Mk 12:31 Hakuna *amri* nyingine iliyo kubwa kuliko hizi
Yoh 13:34 *amri* mpya, kwamba mpendane
AMRI KUMI, Kut 34:28 aliandika zile *Amri Kumi*
AMRIWA, Ayu 23:12 nimeyathamini kuliko *niliyomriwa*
AMSHA, Yoh 11:11 ninasafiri kwenda *kwamwasha*
ANA, Lu 2:36, 37 nabii wa kike *Ana*, miaka 84
ANANIA, Mdo 5:1 *Anania*, na Safira mke wake
ANASA, Ufu 18:7 kuishi katika anasa isiyu na *aibu*
ANAWAJALI, 1Pe 5:7 *anawajali* nanyi
ANDAA, 1Ti 5:8 ikiwa yeyote *hawaandali* watu wake
ANDIKO, 2Ti 3:16 Kila *Andiko* limeongozwa na roho
ANGALIA, Efe 5:15 *kuangalia* sana jinsi mnavyotembea
ANGAMIZA, 2Pe 3:7 *kuangamiza*, wasiomwogopa Mungu
ANGUKA, Met 24:16 mwadilifu, *kuanguka* mara saba
Mhu 4:10 mmoja wao *akianguka*, mwenzake anaweza
1Ko 10:12 ajihadhari asije *akaanguka*
APA, Mwa 22:16 *Naapa* kwa nafsi yangu, asema Yehova
Mt 5:34 *Msiape* kamwe kwa mbingu
APOLO, Mdo 18:24 *Apolo* mwanamume mwenye ufusaha
ARARATI, Mwa 8:4 safina ikatua kwenye mlima *Ararati*
AREOPAGO, Mdo 17:22 Paulo akasimama *Areopago*
ARTEMI, Mdo 13:4 wakimote: *Artemi* ni mkuu!
ASALI, Kut 3:8 nchi inayotirikiwa mazima na *asali*
Met 25:27 Si vizuri kula *asali* nyingi mno
ASILI, Law 18:23 kunukiwa sheria ya *asili*
Ro 1:26 wanawake walibadili matumizi yao ya *asili*
Ro 1:27 wanume waliacha matumizi ya *asili* ya
ASIYEAMINI, 1Ko 7:12 mke *asiyeamini* na anakubali
ASIYEOONEKANA, Ebr 11:27 ona Yule *asiyeeonekana*
ASIYE SAFI, Ayu 14:4 mtu safi kutokana na *asije safi*
AYUBU, Ayu 1:9 Je, *Ayubu* anamwogopa Mungu bure?
Yak 5:11 Mmesikia uvumilivu wa *Ayubu*
AZAZELI, Law 16:8 Haruni atapiga kura kwa *Azazeli*

B

BAALI, Yer 19:5 kuwatekeza wana kwa *Baali*
BABA, Mwa 2:24 atamwacha *baba* yake na mama yake
Zb 2:7 Leo nimekuwa *baba* yako
Zb 89:26 Wewe ni *Baba* yangu, Mungu wangu
Zb 103:13 *baba* anavyoonyesha wana rehema
Isa 9:6 Jina lake litakuwa, *Baba* wa Milele
Mt 6:9 *Baba* yetu uliye mbinguni
Mt 23:9 msimwite mtu yeyote *baba* yenu duniani
Lu 2:49 ninapaswa kuwa katika nyumba ya *Baba*
Lu 15:20 *baba* yake akakimbia, akakumbaba

Yoh 5:20 *Baba* humwonyesha Mwana yote
 Yoh 10:30 Mimi na *Baba* ni kitu kimoja
 Yoh 14:6 Hakuna mtu anayukuja kwa *Baba* bila
 Yoh 14:9 ameniona, amemwona *Baba* pia
 Yoh 14:28 *Baba* ni mkuu kuliko mimi
 Yoh 14:28 mngeshangilia ninaenda kwa *Baba*
BABELI, Mwa 11:9 lilitiwa *Babeli*, kwa sababu
BABILONI, Yer 51:6 Kimbieni kutoka *Babiloni*
 Yer 51:30 Mashujaa wa *Babiloni* hawapigani
 Yer 51:37 *Babiloni* litakuwa marundo ya
 Ufu 17:5 *Babiloni* Mkuubwa, mama wa
 Ufu 18:2 *Babiloni* Mkuubwa ameaunguka
BADILIKA, Mal 3:6 mimi ni Yehova; *sibadiliki*
BADILISHANA, Mt 16:26 *abadilishane* uhai na nini?
BAHARI, Kut 14:21 kukawa na nchi kavu katika *bahari*
 Isa 57:20 waovu ni kama *bahari*
BAHATI, Isa 65:11 mungu wa *Bahati* Njema
BAKI, Mt 14:20 wakakusanya vipande *vilibyobaki*
BALAAMU, Hes 22:28 punda akamuliza *Balaamu*
BAMBA LA KIFUANI, Efe 6:14 *bamba la kifuani*
BARABARA, Mt 7:14 *barabara* ya uzima, ndogo
 Mt 13:4 mbegu zikaanguka kando ya *barabara*
BARAKA, Kum 30:19 nimeweka *baraka* na laana
 Met 10:22 *Baraka* ya Yehova hutajirisha
 Mal 3:10 kuwamwagia *baraka* msikose chochote
 Ro 12:14 *kuwabariki* wanaowatesa
BARIKI, Mwa 1:28 Mungu *akwabariki*
 Mwa 32:26 Sitakuacha mpaka *unibariki*
 Hes 6:24 Yehova na *awabariki*
 Amu 5:24 *Amebarikiwa* sana Yaeli
 Lu 6:28 *kuwabariki* wale wanaowalaani
 Yoh 12:13 *Amebarikiwa* anayukuja katika jina
BARNABA, Mdo 9:27 *Barnaba* akamsaidia
BARUKU, Yer 45:2 Yehova asema kukuhusu, *Baruku*
BATH-SHEBA, 2Sa 11:3 *Bath-sheba*, mke wa Uria
BATIZA, Mt 3:13 Yesu akaja *batizwe* na Yohana
 Mt 28:19 mkafanye wanafuzi, *mkwabatiza*
 Lu 3:3 *wabatizwe* kuonyesha wametubu
 Mdo 2:41 *wakabatizwa*, karibu watu 3,000
 Mdo 8:36 ni nini kinachoniua *kubatizwa*?
BAYA, Tit 2:8 hawana jambo lolote *baya* la kusema
BEBA, Ro 15:1 tunapaswa *kubeba* udhafu
BEGA, Sef 3:9 Wamtumieki *bega* kwa *bega*
BEI, 1Ko 7:23 Mlinunuliwa kwa *bei*
BELSHAZA, Da 5:1 *Belshaza* alifanya karamu kubwa
BEMBELEZA, Met 29:21 Mtumishi *akibembeleza*
BETHELI, Mwa 28:19 akapaita mahali hapa *Betheli*
BETHEHEMU, Mik 5:2 *Bethlehemu* Ephrata
BEZALELI, Kut 31:2 nimemchagua *Bezaleli*
BIASHARA, Mt 22:5 wakaenda kwenye *biashara* zao
 Yak 4:13 tutafanya *biashara* na kupata faida
BIBI HARUSI, Ufu 21:9 Nitakuonyesha *bibi harusi*
BIDII, Zb 69:9 *Bidii* ya nyumba yako imenila
 Met 10:4 mikono yenye *bidii* huleta utajiri
 Met 12:27 *bidii* ni hazina ya mtu yenye thamani
 Met 21:5 Mipango ya wenye *bidii* hufanikiwa
 Isa 37:32 *Bidii* ya Yehova wa majeshi itatenda
 Ro 10:2 wana *bidii* kwa ajili ya Mungu
 Ro 12:11 Iweni yenye *bidii*, msiiwe wavivu
 Tit 2:14 wenye *bidii* katika matendo mema
 Ebr 6:11 kila mmoja wenu uwa na *bidii* ileile
BINTI, Lu 8:49 *Binti* yako amekufa
BORA, Flp 2:3 mwaone wengine kuwa *bora*
BORA ZAIDI, 1Ko 12:31 njia iliyo *bora zaidi*
BUBU, Isa 35:6 ulimi wa *bubu* utapiga vigelegele
BURE, Isa 65:23 Hawatafanya kazi ya *bure*
 Mt 10:8 Mlipokea *bure*, toeni *bure*
 Mt 15:9 Wao huniabu *bure*
 1Ko 15:58 kazi yenu si ya *bure* kwa *Bwana*
 Ufu 22:17 yeyote achukue maji ya uzima *bure*
BURUDISHA, Mt 11:28 Njooi *nitawburudisha*
 Mdo 3:19 majira yenye *kurudisha* yaje
BUSARA, Mt 24:45 mtumwa mwaminifu, *busara*
BUSTANI, Mwa 2:15 akamweka katika *bustani* ya Edeni
BUSU, Lu 22:48 unamsaliti kwa *busu*?
BWANA, Kum 10:17 Yehova ni *Bwana* wa mabwana
 Mt 7:22 *Bwana, Bwana*, je, hatukuwa unabii
 Mt 9:38 mwombeni *Bwana* awatome wafanyakazi

Mt 22:44 Yehova alimwambia *Bwana* wangu
 Ro 6:14 dhambi haipaswi kwa *Bwana*
 Ro 14:4 *Bwana* wake husimama au kuanguka
 1Ko 7:39 huru kuolewa katika *Bwana* tu
 Kol 4:1 ninyi pia mna *Bwana* mbinguni

C

CHACHU, Mt 13:33 Ufalme wa mbinguni kama *chachu*
 1Ko 5:6 *chachu* kidogo huchachisha donge lote
CHAFU, Ro 12:27 wanaume wakitenda *machafu*
 Efe 5:4 wala mizaha *machafu*
 Kol 3:8 ondoeni maneno *machafu*
CHAFUA, Eze 39:7 jina langu takatifu *lichafuliwe* tena
CHAGUA, Kum 30:19 lazima *chagua* uzima
 Yos 24:15 *chagueni* mtakayemtumikia
 Ro 9:11 *kuchagua* hutegemea Yule ambaye
CHAKAA, 2Ko 4:16 mtu tuliye kwa njia *anachakaa*
CHAKULA, Zb 145:15 Unawapa *chakula* katika majira
 Mt 24:7 upungufu wa *chakula*
 Mt 24:45 *chakula* wakati unaofaa
 Yoh 4:34 *Chakula* changu ni kufanya mapenzi ya
 Yoh 6:27 Msifanye kazi *chakula* kinachoharibika
 Mdo 14:17 akiwapa mvua, akiwashibisha *chakula*
 1Ko 8:13 ikiwa *chakula* kinamkwaza ndugu
CHAKULA KIGUMU, Ebr 5:14 *chakula kigumu*
CHALE, Law 19:28 msijianchiye *chale*
CHANZO, Zb 36:9 Wewe ndiye *chanzo* cha uhai
CHEKA, Mwa 18:13 Kwa nini Sara *amecheka*?
 Zb 2:4 anayeketi mbinguni *atacheka*
CHEKWA, Yer 20:7 Nimekuwa kita *chukekwa*
CHELEWA, Hab 2:3 *Hayatachelewa*
CHEMA, Mwa 1:31 kila kitu alichoumba *chikemuwa chema*
CHEMCHEMI, Yer 2:13 Wamenachika, *chemchemi* ya maji
CHEO, Mdo 1:20 achukue *cheo* chake cha uangalizi
CHETI, Mdo 12:41 amwandikiye *cheti* cha talaka
 Mt 19:7 kwa nini Musa aliagiza kutoa *cheti*
CHIPUKIZI, Yer 23:5 nitakapomwinulia Daudi *chipukizi*
CHOCHEA, Flp 2:13 Mungu *anawachoea*
CHOKA, Met 25:25 maji baridi kwa niji *ilyichoka*
 Isa 40:28 *hachoki* kamwe, haishiwi na nguvu
 Isa 40:29 humpa nguvu mtu *ilyichoka*
 Isa 40:31 Watatembea na *hawatachoka*
 Isa 50:4 kumjibi *ilyichoka* neno linalofaa
 Gal 6:9 tutavuna ikiwa *hatutachoka* kabisa
 Ebr 12:3 *msichoke* na kukata tamaa
CHOKOZEKA, 1Ko 13:5 [upendo] *hauchozeki*
CHOMA, Zek 12:10 watamtazama yule *waliyemchoma*
CHOMBO, Mdo 9:15 mtu huyu ni *chombo*
 Ro 9:21 *chombo* cha matumizi ya kuheshimika
CHONGEA, 1Ko 4:13 *tunapochongewa* tunajibu kwa
CHOSHA, Mal 1:13 Tazama! *Inachosha* kwelikweli!
CHOZI, Ufu 21:4 atafuta kila *chozi* kutoka katika
CHUI, Isa 11:6 *chui* atalala pamoja na mwanambuzi
 Da 7:6 mnyama mwingine, kama *chui*
CHUKIA, Law 19:17 *Usimchukie* ndugu yako moyoni
 Zb 45:7 Ulipenda uadilifu na *kuchukia* uovu
 Zb 97:10 mnaompenda Yehova, *chukieni* maovu
 Met 6:16 vitu sita ambavyo Yehova *anachukia*
 Met 8:13 Kumuogopa Yehova ni *kuchukia* uovu
 Amo 5:15 *Chukieni* maovu, pendeni mema
 Mt 24:9 *mtachukiwa* kwa sababu ya
 Lu 6:27 kuwatenda mema wale *wanaowachukia*
 Yoh 7:7 Ulimwengu *unachukia* kwa kutoa
 Yoh 15:25 *Walinchukia* bila sababu
 Ro 12:9 *Chukieni* maovu; shikamneni na mema
 1Yo 3:15 *anayemchukia* ndugu yake ni muujaji
CHUMA, Met 27:17 Kama *chuma* kinavyonona *chuma*
 Isa 60:17 badala ya *chuma* nitaleta fedha
 Da 2:43 *Chuma* kisivyochanganyika na udongo
CHUMVI, Mwa 19:26 akawa nguzo ya *chumvi*
 Mt 5:13 Ninyi ndio *chumvi* ya dunia
 Kol 4:6 Maneno yaliyokolezwa *chumvi*
CHUNGA, Mdo 20:28 *mlichunge* kutaniko la *bustani*
 1Pe 5:2 *Lichungeni* kundi la Mungu
CHUNGU, Met 6:6 Mwende *chunga*, ewe mvivu
 Met 30:25 *Chungu* wanataryisha *chakula*
CHUNGULIA, 1Pe 1:12 Malaika, *kuchungulia*
CHUNGUZA, Met 21:2 Yehova *huichunguza* mioyo

Met 25:2 utukufu wa wafalme, *kuchunguza* jambo
Mdo 17:11 *wakiyachunguza* Maandiko
1Ko 11:28 acheni mtu *ajichunguze* mwenyewe

D

DADA, Kum 27:22 anayefanya ngono na *dada* yake
DAIMA, Da 6:16 Mungu wako unayemtumikia *daima*
DAIWA, Lu 12:48 alipewa engeji *atadaiwa* mengi
DAKTARI, Lu 5:31 wenye afya hawahitaji *daktari*
DAMU, Mwa 9:4 *damu*—hampaswi kula
Law 7:26 Hampaswi kula *damu* yoyote
Law 17:11 uhai umo katika *damu*
Law 17:13 imwage *damu* na kuifunika kwa udongo
Zb 72:14 *damu* yao ina thamani machoni pake
Eze 3:18 *damu* yake nitaiddi kutoka kwako
Mt 9:20 mtrikirio wa *damu* kwa miaka 12
Mt 26:28 inamaanisha *damu* yangu ya agano
Mt 27:25 *Damu* yake na iwe juu yetu na watoto wetu
Mdo 15:29 kuendelea kujipusha na *damu*
Mdo 20:26 sina hatia ya *damu* ya mtu yeyote
Mdo 20:28 alilinnuna kwa *damu* ya Mwana wake
Efe 1:7 tunaachiliwa huru kupitia *damu* ya huyo
1Pe 1:19 ilikuwa kwa *damu* yenye thamani ya Kristo
1Yo 1:7 *damu* ya Yesu hutusafisha dhambi
Ufu 18:24 ilipatikana *damu* ya watakatifu
DANSI, Amu 11:34 binti akataka akicheza *dansi*
DAUDI, 1Sa 16:13 Samweli akamtia mafuta *Daudi*
Lu 1:32 kiti cha ufalme cha *Daudi* baba yake
Mdo 2:34 *Daudi* hakupanda mbinguni
DAWA, Met 17:22 Moyo wenye shangwe ni *dawa*
DAWA YA MACHO, Ufu 3:18 *dawa* yako ya *macho* ili uone
DENI, Ro 1:14 nina *dani* kwa Wagiriki
Ro 13:8 Msiwe na *dani*, isipokuwa kupendana
DHABIHU, 1Sa 15:22 Kutii ni bora kuliko *dhabihu*
2Sa 24:24 *dhabihu* ambazo hazingharimu
Zb 40:6 Hukutamani *dhabihu* na toleo
Zb 51:17 *Dhabihu* zinazompendeza Mungu ni roho
Met 15:8 *Dhabihu* ya waovu huchukiza Yehova
Isa 1:11 Nimotosheka na *dhabihu* zenu za kuteketezwa
Ho 6:6 sipendeziwa na *dhabihu* nzima
Ro 12:1 miili yenu, *dhabihu* iliyo hai
Ebr 13:15 tumtolee Mungu *dhabihu* ya sifa
DHABIHU YA DAIMA, Da 11:31 *dhabihu* inayotolewa *daima*
Da 12:11 kuondolewa *dhabihu* inayotolewa *daima*
DHABAHUBU, Eze 7:19 *dhababu* yao huitawaokoa
Da 3:1 Nebukadnezar atengeneza sanamu ya *dhababu*
DHAIFU, 1Ko 1:27 Mungu alivichagua vitu *dhaifu*
2Ko 12:10 ninapokuwa *dhaifu*, nina nguvu
1Th 5:14 wasaidieni *dhaifu*, iweni na subira
1Pe 3:7 chombo *dhaifu* zaidi, mwanamke
DHAMBHI, Mwa 4:7 *dhambi* inakunyemelea mlangoni
Mwa 39:9 uovu huu nimtendee Mungu *dhambi*?
2Sa 12:13 Daudi: Nimemtendee Yehova *dhambi*
1Fa 8:46 hakuna asiyetenda *dhambi*
Zb 32:1 ana furaha, ambaye *dhambi* imefunikwa
Zb 38:18 Nilihangaishwa na *dhambi* yangu
Isa 1:18 Ingawa *dhambi* zenu ni nyekundu
Isa 38:17 Umetupa *dhambi* nyuma yako
Isa 53:12 Aliibeba *dhambi* ya watu wengi
Yer 31:34 sitaikumbuka tena *dhambi* yao
Eze 33:14 mwovu akiacha *dhambi*
Mt 18:15 ndugu akitenda *dhambi*, nenda
Mk 3:29 kufuru roho, *dhambi* ya milele
Yoh 1:29 Mwanakondoo anayeondoa *dhambi*
Mdo 3:19 tubuni, mgeuke, *dhambi* zifutwe
Ro 3:23 wamefanya *dhambi* na kupungukiwa
Ro 3:25 akisamehe *dhambi* za zamani
Ro 5:12 kupitia mtu mmoja *dhambi* ililingia
Ro 6:14 *dhambi* haipaswi kuwa bwana juu yenu
Ro 6:23 mshahara wa *dhambi* ni kifo
1Ti 5:24 *Dhambi* za wengine hujulikana baadaye
Yak 4:17 kutofanya yaliyo sawa ni *dhambi*
Yak 5:15 ikiwa amefanya *dhambi*, atasamehewa
1Yo 1:7 *damu* ya Yesu hutusafisha *dhambi*
1Yo 2:1 akitenda *dhambi*, tuna msaidizi
1Yo 5:17 Ukosefu wa uadilifu ni *dhambi*

DHAMIRI, Ro 2:15 *dhmiri* yao ikiwatolea ushahidi
Ro 13:5 pia kwa sababu ya *dhmiri* yenu
1Ko 8:12 kuiumiza *dhmiri* yao dhifu
1Ti 4:2 *dhmiri* zao zimetwa alama
1Pe 3:16 Iweni na *dhmiri* njema
1Pe 3:21 ombi la kupata *dhmiri* njema
DHARAU, Isa 53:3 Alidharauliwa na kuepukwa
DHIBITI, Met 10:19 anayedhibiti midomo yake
Met 16:32 anayedhibiti hasira yake ni bora kuliko
1Th 4:4 kujua jinsi ya kuudhibiti mwili wake
DHIDI, Ro 8:31 nani atakuwa dhidi yetu?
DHIHAKI, Met 27:11 niweze kumjibu yule anayenidhihaki
Lu 18:32 atadhihakiwa, na kutemewa mate
Lu 22:63 wakaanza kumdhihaki na kumpiga
Gal 6:7 Mungu si wa kudhihakiwa
DHIKI, Mt 24:21 *dhiki* kuu ambayo hajawahi kutokea
Mdo 14:22 tuingie katika Ufalme kupitia *dhiki*
Ro 5:3 tushangilie, *dhiki* hutokeza uvumilivu
Ro 12:12 Vumilieni chini ya *dhiki*
1Ko 7:28 wanaoaa wana *dhiki* katika mwili
2Ko 4:17 ingawa *dhiki* ni ya muda mfupi
Ufu 7:14 wale wanaotoka katika ile *dhiki* kuu
DINA, Mwa 34:1 *Dina* alizoea kwenda kuwatembelea
DINARI, Lu 7:41 mmoja alikuwa na deni la *dinari* 500
DIRISHA, Mdo 20:9 Eutiko alikuwa ameketi *dirishani*
DIVAI, Law 10:9 msinywe *divai* mnapingia
Zb 104:15 *divai* inafanya moyo ushangilie
Met 20:1 *Divai* ni mdhihaki, kileo ni vurugu
Met 23:31 Usitazame rangi nyekundu ya *divai*
Mhu 10:19 *divai* hufanya maisha yafurahishe
Isa 25:6 Karamu ya *divai* bora, iliyoichujwa
Ho 4:11 *divai* huondoa kichocho cha
Yoh 2:9 maji yaliyogezwa kuwa *divai*
1Ti 5:23 *divai* kidogo kwa ajili ya tumbo
DOGO, Lu 16:10 mwaminifu katika dogo ni
DORKASI, Mdo 9:36 aliyetwa Tabitha, *Dorkasi*
DRAKMA, Lu 15:8 mwanamke aliye na *drakma*
DUA, 1Ti 2:1 *dua*, sala zitolewe kwa wote
Ebr 5:7 Kristo alitoa *dua* na maombi
Yak 5:16 *Dua* ya mtu mwaadilifu
DUARA, Isa 40:22 anayekaa juu ya *duara* ya dunia
DUBU, 1Sa 17:37 aliyeniokoa kutoka kwa *dubu*
Isa 11:7 Ng'ombu na *dubu* watakuwa pamoja
DUMU, 1Yo 2:17 mapenzi ya Mungu, *anadamu* milele
DUNI, Zb 119:141 Mimi ni *duni* na mwenye kudharauliwa
DUNIA, Mwa 1:28 mujiage *dunia* na kuitiisha
Kut 9:29 *dunia* ni ya Yehova
Ayu 38:4 nilipoweka misingi ya *dunia*?
Zb 37:11 wapole wataimiliki *dunia*
Zb 37:29 Waadilifu wataimiliki *dunia*
Zb 104:5 *dunia* haitasogezwa kutoka mahali pake
Zb 115:16 *dunia* amewapa wanadamu
Met 2:21 ni wanyoofu tu wataokaa *duniani*
Isa 45:18 *dunia* iliumbwa ili ikaliwe
Mt 5:5 wapole watairithi *dunia*

E

EDENI, Mwa 2:8 Mungu akapanda bustani kule *Edeni*
EFESO, 1Ko 15:32 wanyama huko *Efeso*
ELEWA, Ne 8:8 wakawasaidia *kuelewa* yaliyosomwa
Ayu 6:24 Nisaidieni *kuelewa* kosa langu
Zb 119:27 Nifanye *nielewa* maagizo yako
ELEZA, Yoh 1:18 mungu mzaliwa pekee *ameeleza*
ELFU, Zb 91:7 *Elfu* moja wataangka gando yako
Isa 60:22 Mdogo atakuwa *elfu*
2Pe 3:8 siku moja ni kama miaka *elfu*
ELI, 1Sa 1:3 Wana wa *Eli* walikuwa makuhani
ELIMU, Mdo 4:13 watu wasio na *elimu* na wa kawaida
ELIYA, Yak 5:17 *Eliya*, mtu mwenye hisia kama zetu
ENEO, Ro 15:23 *eneo* ambalo halijaguswa
ENOKO, Mwa 5:24 *Enoko* alielelelea kutembea na Mungu
EPUKA, Isa 53:3 Alidharauliwa na kuepukwa
ESAU, Mwa 25:34 *Esau* akaidharau haki yake ya kuzaliwa
Ebr 12:16 asiyeathamini, kama *Esau*
EUODIA, Flp 4:2 Ninawahimiza *Euodia* na Sintike
EZRA, Eze 7:11 *Ezra* aliyekua kuhani na mwandishi

F

FADHILI, Met 11:17 mwenye *fadhili* hujunfaisha
Met 31:26 Sheria ya *fadhili* kwenye ulimi wake
Yoh 1:17 *fadhili* zisizostahiliwa kupitia
Mdo 28:2 walitutendea kwa *fadhili* nyingi
1Ko 15:10 *fadhili* zisizostahiliwa hazikuwa za bure
2Ko 6:1 *fadhili* zisizostahiliwa na kukosa kusudi
2Ko 12:9 *Fadhili* zangu zisizostahiliwa zinakutosha
FAFANUA, Ne 8:8 *wakiiafafanua* waziwazi na kueleza
FAHAMU, Lu 15:17 Aliporudiwa na *fahamu* akasema
FAHARI, Met 19:11 ni *fahari* kuachilia kosa
FAIDA, Kum 10:13 kushika amri kwa *faida* yenu
Met 14:23 kazi ngumu ina *faida*
Met 15:27 *faida* isiyu ya haki huleta taabu
Isa 48:17 Ninayekufundisha ili *ujifaidi*
Mdo 20:20 kuwaambia jambo lenye *faida*
1Ko 7:35 kwa *faida* yenu wenyewe
1Ko 10:24 kutafuta, si *faida* yake mwenyewe
1Ko 13:5 [upendo] hautafuti *faida* zake wenyewe
2Ko 7:2 hatujamdanganya yeyote ili tupate *faida*
Flp 2:4 si *faida* zenu wenyewe, bali pia *faida*
Flp 2:21 wengine wanatufuta *faida* zao wenyewe
2Ti 3:16 limeongozwa na roho ni lenye *faida*
FALME, Mt 4:8 Ibilisi akamwonyesha *falme* zote
FALSIFA, Kol 2:8 mateka kupitia *falsafa*
FAMILIA, Efe 3:15 kila *familia* mbinguni na duniani
FANIKISHA, Yos 1:8 utakapofanikisha njia yako
FANIKIWA, 1Fa 2:3 utafanikiwa katika kila jambo
2Ny 20:20 imani katika manabii, *mtafanikiwa*
Zb 1:3 kila jambo analofanya *litafanikiwa*
Isa 55:11 neno langu *litafanikiwa* hakika
FANYA, Ro 7:15 *sifanyi* kile ninachotaka, bali
FANYA KAZI, Ro 12:4 viungo *havifanyi* *faida* ileile
Efe 4:16 kila kiungo kinapofanya kazi vizuri
FARAJA, Zb 94:19 *Ulinifariji* na kunibembeleza
Isa 49:13 Yehova amewafariji watu wake
Yer 31:15 Raheli amekataa *kufarijiwa*
Mt 5:4 wanaoombeza, *watafarijiwa*
2Ko 1:3 Mungu wa faraja yote
2Ko 1:4 ili tuweze *kuwafariji* wengine
FARASI, Ufu 6:2 *farasi* mweupe, yule aliyeketi
Ufu 19:11 tazamal *farasi* mweupe
FARIJI, Ayu 2:11 waenda kumpa pole na *kumfariji* Ayubu
Isa 61:2 *Kuwafariji* wote wanaoombeza
Ro 15:4 kupitia *faraja* kutoka kwa Maandiko
1Th 2:11 endelea kumhimiza, *kumfariji*
FEDHA, Met 2:4 kuatufata kama *fedha*
Eze 7:19 Watatupa *fedha* yau barabarani
Sef 1:18 *Fedha* wala dhahabu haitawaokoa
FICHA, Lu 8:17 lolote *lililofichwa* litafunuliwa
FIDIA, Zb 49:7 hakuna anayeweza kumpa Mungu *fidia*
Mt 20:28 Mwana alikuja kutoka uhai wau *fidia*
Ro 8:23 kuachiliwa kwenye miili kupitia *fidia*
FIKIRA, Nah 1:7 Anawakazia *fikira* wanaotafuta kimbilio
2Ko 10:5 kila *fikira* inatii Kristo
FIKIRI, Ro 12:3 *asijifikirie* kuliko iliyo lazima
FILIPO, Mdo 8:26 malaika akamwambia *Filipo*
Mdo 21:8 *Filipo*, mmoja wa wale saba
FIMBO, Mwa 49:10 *Fimbo* ya ufalme haitaondoka Yuda
2Zb 2:1 Utawavunja kwa *fimbo* ya chuma
Met 13:24 anayezuia *fimbo* anamchukia mwana
Ufu 12:5 atakayechungu mataifa yote kwa *fimbo*
FINEHASI, Hes 25:7 *Finehasi* alipoona jambo hilo
FINYANGA, Ro 12:2 *kufinyangwa*, mfumo huu
1Pe 1:14 acheni *kufinyangwa* na tamaa
FUATA, Mt 4:20 wakaziacha nyavu zao na *kumfuata*
Yoh 10:27 Kondoo wangu husikiliza na *kunifuata*
Ufu 14:4 *kumfuata* Mwanakondoo popote
FUATILIA, Ro 14:19 *tufuatilie* yanayoleta amani
FUMBA, Kum 15:7 *kumfumba* mkono ndugu yenu
FUNDISHA, Amu 13:8 Manoa, *tufundishe* kumlea
Ezr 7:10 Ezra alitayarisha moyo *kufundisha*
Zb 32:8 *kukufundisha* njia unayopaswa kufuta
Zb 14:3:10 *Nifundishe* kufanya mapenzi yako
Met 9:9 *Mfundishe* mwenye hekima, atazidi
Isa 48:17 *Ninayekufundisha* ili *ujifaidi*
Yer 31:34 *hawatafundishana* mtu na ndugu yake

Mt 7:28 njia yake ya *kufundisha*
Mt 7:29 *akiwafundisha* kama mtu mwenye mamlaka
Mt 15:9 *wanafundisha* amri za wanadamu
Mt 28:20 *kuwafundisha* kushika mambo yote
Yoh 7:16 Mambo *ninayafundisha* si yangu
Ro 2:21 wene *unayemfundisha* mtu mwingine
Ro 15:4 yaliandikwa ili *kutufundisha*
1Ti 2:12 Simruhusu mwanamke *afundishe*
FUNDISHA, Isa 54:13 *watafundisha* na Yehova
Yoh 7:15 ingawa *hajafundisha* shuleni
FUNGA, Mwa 22:9 *Akamfunga* isaka mwanawe
Isa 61:1 *kuufunga* majeraha ya waliowinjika moyo
Eze 34:16 aliyejeruhiwa *nitamfunga*
Mt 16:19 utakalofunga duniani limefungwa
FUNGU, Omb 3:24 Yehova ni *fungu* langu
Da 12:13 utasimama kwa ajili ya *fungu* lako
FUNGUU, Mt 18:18 mambo *mtakayofunga* duniani
FUNGUO, Mt 16:19 Nitakupa *fungu* za Ufalme
Ufu 1:18 nina *fungu* za kifo na za Kaburi
FUNIKA, Mt 28:13 Anayefunika makosa yake
1Ko 11:6 ikiwa mwanamke *hajifuniki*
FUNIKA DHAMBI, Law 16:34 *kufunika dhambi* kila mwaka
FUNUA, Mt 11:25 *umeyafunua* kwa watoto wadogo
1Ko 2:10 Mungu ameyafunua kwetu kupitia roho
FUNULIWA, Ro 8:19 *kufunuliwa* kwa wana
Efe 3:5 siri imefunuliwa kwa mitume na manabii
FURAHA, Zb 32:1 Mwenye *furaha*, dhambi imefunikwa
Zb 37:4 Pata *furaha* tele katika Yehova
Zb 94:12 Mwenye *furaha* ni mtu unayemrebekisha
Zb 144:15 Wenyewe *furaha*, Mungu wao ni Yehova!
Mt 5:3 Wenyewe *furaha* hutambua uhitaji
Mdo 20:35 *furaha* katika kutoa kuliko kupokea
1Ti 1:11 habari njema ya Mungu mwenye *furaha*
FURAHIA, Zb 149:4 Yehova anawafuraha watu wake
Eze 18:32 Mimi *sifurahii* kifo cha mtu yeyote
FURAHIA, Zb 40:8 *ninafurahia* kufanya mapenzi yako
Mhu 2:24 kuliko *kufurahia* kazi yake ngumu
FUTA, Mdo 3:19 ili dhambi zenu *zifutwe*

G

GABRIELI, Lu 1:19 *Gabrieli*, ninayesimama karibu
GAMALIELI, Mdo 22:3 nililelimishwa na *Gamalieli*
GEHAZI, 2Fa 5:20 *Gehazi*, nitakimbia na kumfuata
GEHENA, Mt 18:28 nafsi na mwili katika *Gehena*
GEREZA, Mt 25:36 Nilikuwa *gerezani* mkanitembelea
Mdo 5:19 malaika akafungua milango ya *gereza*
Mdo 12:5 Petro alikuwa *gerezani* lakini kutaniko
Ebr 13:3 Wakumbukeni wale wali *gerezani*
Ufu 2:10 Ibilisi ataendelea kuwatupa *gerezani*
GHAFLA, Lu 21:34 siku ile iwakute *ghafila*
GHARAMA, Lu 14:28 kuhesabu *gharama*
Lu 14:28 keti na kuhesabu *gharama*
1Ko 9:18 niitoe habari njema bali *gharama*
GHARIKA, Mwa 9:11 hawataangamizwa kwa *gharika*
Mt 24:38 kabla ya *Gharika*, wakila na
2Pe 2:5 alipoleta *gharika* juu ya ulimwengu
GHASIA, Mdo 17:5 kikundi chenye *ghasia*
GIBEONI, Yos 9:3 Wakaaji wa *Gibeoni* walisikia pia
GIDEONI, Aumu 7:20 Upanga wa Yehova na wa *Gideoni!*
GIZA, Isa 60:2 *giza* litafunika dunia
Yoe 2:31 Juu litawia *giza*
Mt 4:16 wanaokaa katika *giza* waliona nuru
Yoh 3:19 watu wamepanda *giza*
Efe 4:18 Wako *gizani* kiakili
1Pe 2:9 aliyewaita kutoka katika *giza*
GOLGOTHA, Yoh 19:17 Fuvu la Kichwa, au *Golgotha*
GOLIATHI, 1Sa 17:4 shujaa, alitwaga *Goliathi*
GOMORA, Mwa 19:24 kiberti na mtoto juu ya *Gomora*
GURUDUMU, Eze 1:16 *gurudumu* ndani ya *gurudumu*
GUSA, Met 6:29 *anayemgusa* mwanamke atadhahiwa
Isa 52:11 *msiguse* kitu chochote kichafu!
Mt 8:3 *akamgusa* na kusema: Ninataka!
2Ko 6:17 mwache *kgusa* kitu kichafu

H

HABARI, Kut 23:1 Usieneze *habari* za uwongo
Lew 5:1 shahidi amekataa *kutoa habari*
Has 14:36 wakaleta *habari* mbaya kuhusu nchi

Zb 112:7 Hataogopa *habari* mabaya
 Met 25:25 *habari* njema kutoka nchi ya mbali
 Da 11:44 *habari* zitamhangaiha
 2Ko 6:8 kupitia *habari* mabaya, *habari* nzuri
HABARI NJEMA, Isa 52:7 miguu ya anayeleta *habari njema*
 Mt 24:14 *habari njema* itahubiriwa
 Lu 4:43 lazima pia nitangaze *habari njema*
 Ro 1:16 sioneni alibu *habari njema*
 1Ko 9:16 ole wangu nisipotangaza *habari njema!*
 1Ko 9:23 ninafanya yote kwa ajili ya *habari njema*
HADESI, Angalia KABURI.
HAI, Da 6:26 yeye ndiye Mungu aliye *hai*
 Lu 20:38 Mungu wa walio *hai*, wote wako *hai*
 1Th 4:15 sisi tulio *hai* ambao tutabaki
 Ebr 4:12 neno la Mungu liko *hai* nalo ni lenye nguvu
 1Pe 3:18 akafanywa kuwa *hai* katika roho
HAKI, Kum 32:4 Mungu asiye na ukosefu wa *haki*
 Ayu 34:12 Mweza-Yote hapotoshi *haki*
 Ayu 40:8 Je, utatilia shaka *haki* yangu?
 Zb 37:28 Yehova anapenda *haki*
 Met 15:27 Mtu anayepata faida isiyo ya *haki*
 Met 29:4 Kwa *haki* mfalme huleta uthabiti nchini
 Mhu 5:8 usishangazwe ukiona *haki* ikiikiuwa
 Isa 32:1 wakuu watatawala kwa *haki*
 Eze 21:27 yule aliye na *haki* ya kisheria atakapokuja
 Mik 6:8 utekeleze *haki*, uthamini sana ushikamanifu
 Lu 18:7 hatawatendea *haki* watu wake?
 Mdo 28:4 *Haki* haikumruhusu aendeleo kuishi
 Ro 9:14 Mungu ana ukosefu wa *haki*? La hashah!
 1Ko 7:3 Mume na ampe mke wake *haki* yake
 1Pe 2:19 inakubalika akiteseka isiyo *haki*
HAKIKISHA, Flp 1:10 *mhakikishe* mambo muhimu
 1Th 5:21 *Hakikisheni* mambo yote
HALALI, 1Ko 6:12 Mambo yote ni *halali* kwangu, lakini
HABERUYA, Angalia MSIFUNI YAH.
HALISI, Yoh 7:28 aliyenituma ni *halisi*
HALI YA CHINI, Isa 2:8 Huminiua mtu wa *hali* ya *chini*
 Zb 41:1 anayemjali mtu wa *hali* ya *chini*
 Isa 57:15 kuihuisha roho ya watu wa *hali* ya *chini*
HAMU, Ro 1:26 *hamu* isiyodhibitiwa yenye kuchukiza ya ngono
 Ro 16:18 watumwa wa *hamu* yao
 Flp 2:13 kuwapa *hamu* na nguvu za kutenda
 Kol 3:5 *hamu* isiyodhibitiwa ya ngono
 1Th 4:5 *hamu* yenye pupa ya ngono
 1Pe 2:2 kuzeni *hamu* ya maziwa ya neno
HANGAIKA, Isa 41:10 *Usihangaika*, mimi ni Mungu wako
 Mt 6:34 *msihangaika* kame kuhusu kesho
 Mt 10:19 *msihangaika* kuwewa mtakalosema
 Lu 12:25 kwa *kuhangaika* anaweza kurefusha uhai?
 1Ko 7:32 ninataka *msihangaika*
 1Ko 7:32 Mwanamume ambaye hajaoa *huhangaika*
 2Ko 11:28 *kuhangaika* makutaniko yote
 Flp 4:6 *Msihangaika* kuhusiana na lolote
HARADALI, Lu 13:19 kama mbeu ya *haradali*
HARAKISHA, Isa 60:22 Mimi, Yehova, *nitaliharakisha*
HARIBU, Eze 21:27 *Nitaliharibu, nitaliharibu, nitaliharibu*
 Ufu 11:18 *kuwaharibu* wale wanaoahiribu dunia
HAR-MAGEDONI, Ufu 16:16 panaitwa *Har-Magedoni*
HASARA, Flp 3:7 nimeviona kuwa *hasara*
HASIRA, Zb 37:8 Acha *hasira* na ghadhabu
 Zb 103:8 Yehova si mwepesi wa *hasira*
 Met 14:17 *anayekasirika* upesi hutenda kipumbavu
 Met 16:32 mtu anayedhibiti *hasira* yake
 Kol 3:8 ondoeni *hasira*, matukano
HASIRA KALI, Met 19:19 mwenye *hasira kali* atalipia
HATARI, Met 22:3 Mtu mwerevu huona *hatari* na kujificha
 Mt 11:26 *hatari* jijini, *hatari* nyikani
 2Ti 3:1 nyakati za *hatari* zilizo ngumu
HATARISHA, Ro 16:4 ambao *wamehatarisha* shingo zao
HATI, Yer 32:12 nikampa *hati* ya ununuzi Baruku
HATIA, Ro 6:7 aliyekufa ameondolewa *hatia*
HATIA YA DAMU, Mdo 20:26 sina *hatia* ya *damu* ya mtu
HATUA, Yer 10:23 mwanadamu hawezi kuongoza *hatua*
 Gal 6:1 mtu akichukua *hatua* isiyofaa
 1Pe 2:21 mfuate *hatua* zake kwa ukaribu
HAYA, Eze 9:6 ninaona *haya* kuinua usi wangu kwako
HAZINA, Met 2:4 kutafuta kama *hazina* zilizofichika
 Met 10:2 *Hazina* zilizopatikana kwa uovu

Mt 6:21 moyo utakuwa mahali ilipo *hazina*
 Mt 13:44 Ufalme kama *hazina* iliyofichwa
 Lu 6:45 mema kwenye *hazina* ya moyo wake
 Lu 12:33 *hazina* isiyounguwa huko mbinguni
 2Ko 4:7 tuna *hazina*, vyombo vya udongo
HEDHI, Law 15:19 *hedhi*, hatakuwa safi kwa siku saba
 Law 18:19 ngono wakati wa *hedhi*
HEKALU, Pia angalia YUMBA
 Zb 11:4 Yehova yumo katika *hekalu* lake
 Zb 27:4 kutazama kwa uthamini *hekalu* lake
 Yer 7:4 *hekalu* la Yehova, *hekalu* la Yehova
 Eze 41:13 Akapima *hekalu*, urefu wa mikono 100
 Mal 3:1 ghafla Bwana atakuja katika *hekalu* lake
 Mt 21:12 akangia *hekaluni* na kuwafukuza
 Yoh 2:19 Libomoeni *hekalu* hili, na kwa siku tatu
 1Ko 3:16 ninini ni *hekalu* la Mungu
HEKIMA, Zb 111:10 Kumwogoa Yehova ni *hekima*
 Zb 119:98 hufanya niwepa na *hekima* kuliko maadui
 Met 2:6 Yehova mwenyewe hutoa *hekima*
 Met 3:7 Usiwe mwenye *hekima* machoni pako
 Met 4:7 *Hekima* jambo muhimu zaidi
 Met 8:11 *hekima* ni bora kuliko marijani
 Met 9:9 Mfundishe mwenye *hekima*, atazidi
 Met 13:20 Anayetembea na wenye *hekima*
 Met 24:3 Nyumba hujengwa kwa *hekima*
 Met 27:11 Uwe na *hekima*, mwanangu
 Mhu 7:12 *Hekima* humifadhi hai yule aliye nayo
 Mhu 10:10 *hekima* husaidia kuleta mafanikio
 Isa 5:21 Ole walio na *hekima* machoni pao
 Mt 11:19 *hekima* huthibitishwa kupitia kazi zake
 Mt 11:25 umewaficha mambo haya wenye *hekima*
 Lu 16:8 wana *hekima* zaidi katika kipitaji chao
 Lu 16:8 wana *hekima* zaidi kuliko wana wa nuru
 Lu 21:15 *hekima* ambayo wapinzani hawataishinda
 Ro 11:33 kina cha utajiri wa Mungu na *hekima*
 1Ko 1:26 si wengi wenye *hekima* kimwili
 1Ko 2:5 imani si katika *hekima* ya wanadamu
 1Ko 2:6 si *hekima* ya watawala wa mfumo huu
 1Ko 3:19 *hekima* ya ulimwengu huu ni upumbavu
 Efe 5:15 mtembee kama watu wenye *hekima*
 Kol 2:3 *Hazina* za *hekima* zimeficha ndani yake
 Yak 1:5 ikiwa yeyote anakosa *hekima*
 Yak 3:17 *hekima* inayotoka juu
HEKIMA INAYOTUMIKA
 Met 2:7 Huwahifadhi *hekima* inayotumika
 Met 3:21 Linda *hekima* inayotumika na uwezo
 Lu 16:8 alitenda kwa *hekima* inayotumika
HEMA, Yos 18:1 kupiga *hema* la mkutano, Shilo
 Zb 15:1 kuwa mgeni katika *hema* lake
 Isa 54:2 refusha kamba za *hema* lake
 2Ko 12:9 nguvu za Kristo kama *hema*
 Ufu 21:3 *Hema* la Mungu liko na wanadamu
HEMA LA IBADA, Zb 78:60 akaliacha *hema* la *ibada*, Shilo
 Zb 84:1 linavyoitua *hema* lake tukufu la *ibada*
HESABIWA, Lu 22:37 *alishesabiwa* na waasi sheria
HESABU, Zb 90:12 Tufundishe *heshabu* siku zetu
HESHIMA, Met 5:9 msiwape wengine *heshima* yenu
 Ro 12:10 kuonyeshana *heshima*, iweni wa kwanza
 1Ti 5:17 wanastahili *heshima* mara mbili
 1Pe 3:2 mwenendo safi na *heshima* kubwa
 1Pe 3:15 kujiteta kwa upole na *heshima* kubwa
HESHIMU, Kut 20:12 *Mheshimu* baba yako na mama yako
 2Sa 12:14 *hukumheshimu* Yehova kamwe
 Met 3:9 *Mheshimu* Yehova kwa vitu vyenye thamani
 Efe 5:33 mke *kumheshimu* mume wake
 Flp 2:29 mwendelee *kuwaheshimu* sana
 1Th 5:12 *waheshimu* wali wanaoasisimamia
HEWA, 1Ko 9:26 nisiwe nikipiga *hewa*
 1Ko 14:9 mtakuwa mkizungumza *hewani*
 Efe 2:2 mtawala wa mamlaka ya *hewa*
HEZEKIA, 2Fa 19:15 *Hezekia* akaanza kusali kwa Yehova
HIARI, Kut 19:8 tuko *tayari* kufanya
 Kut 35:5 aliye na moyo wa kutoa kwa *hiari*
 1Nya 29:17 nimetoa kwa *hiari* vitu hivi vyote
 Zb 110:3 Watu wako watajitoa kwa *hiari*
 1Pe 5:2 Lichungeni kundi kwa *hiari*

HILA, Met 3:32 Yehova humchukia mtu mwenye *hila*

Yer 17:9 Moyo ni wenye *hila* kuliko

Mal 2:15 usimtendee kwa *hila* mke

HISIA, Yak 5:17 Eliya, mtu mwenye *hisia* kama zetu

HITAJI, Mt 6:32 Baba anajua *mnahitaji* vitu hivi vyote

HODI, Mt 7:7 endeleeni kupiga *hodi*, mtafunguliwa

HORI, Lu 2:7 na kumlaza katika *hori*

HOTUBA, Mdo 15:32 wakawatia moyo kwa *hotuba* nyingi

HUBIRI, Mt 24:14 habari njema ya Ufalme *ihubiririwa*

Ro 10:14 watasikiaje bila mtu wa *kuhubiri*?

2Ti 4:2 *Lihubiri* neno; fanya hivyo kwa uhakika

HUDUMA, Mdo 20:24 nimalize mwendo na *huduma*

Ro 11:13 ninaitukuza *huduma* yangu

2Ko 4:1 tuna *huduma* hii kupitia rehema

2Ko 6:3 kosa lisipatikane katika *huduma* yetu

1Ti 1:12 aliniona mwaminifu kwa kunipa *huduma*

2Ti 4:5 timiza kikamilu *huduma* yako

HUDUMU, Da 7:10 maelfu waliendelea *kumhudumia*

Mt 20:28 Mwana wa binadamu alikuja *kuhudumu*

1Pe 4:10 itumieni zawadi *kuhudumiana*

HUISHA, Isa 57:15 *kuihusu* watu wa hali ya chini

HUKOPA, Zb 37:21 Mwovu *wakupa* lakini halipi

HUKUMU, Mhu 8:11 sababu *hukumu* haijatekelezwa

Isa 26:9 *hukumu* zinapotoka kwako kwa dunia

Mt 7:2 kwa *hukumu* mnaoyohukumu, mtaahukumiwa

Lu 6:37 acheni *kuhukumu*, nanyi hamtahukumiwa

Lu 22:30 kuketi kwenye viti *kuyahukumu* makabala 12

Yoh 5:22 amemkabidhi Mwana kazi ya *kuhukumu*

Mdo 17:31 ameweka siku anayokusudia *kuhukumu*

Ro 14:4 Wewe ni nani *umhukumu* mtumishi wa

1Ko 6:2 hamjui watakatifu *watahukumu* ulimwengu?

1Ko 11:29 kunya *hukumu* dhidi yake mwenyewe

2Ko 1:9 tulihisi tumepokea *hukumu* ya kifo

Yak 4:12 wewe ni nani *umhukumu* jirani yako?

1Pe 4:17 *hukumu* kuanza na nyumba ya Mungu

HURU, Yoh 8:32 kweli itawaweka ninyi *huru*

Ro 6:18 miwewe *huru* kutoka katika dhambi

HURUMA, Kut 34:6 Yehova ana rehema na *huruma*

Mt 16:22 Bwana *jihurumie*

Kol 3:12 upendo mwororo wenye *huruma*

1Yo 3:17 naye akataa *kumhurumia*

HUZUNI, Zb 31:10 Maisha yangu yamejaa *huzuni*

Zb 38:6 mchana kutwa kwa *huzuni*

Zb 90:10 miaka imejaa *huzuni*

Mhu 7:3 uso wenye *huzuni* huboresha moyo

Isa 51:11 *Huzuni* na kilio vitakimbia

2Ko 2:7 asilemewe na *huzuni* inayopita kiasi

HUZUNIKA, Flp 2:26 [Epafrodito] amehuzunika

1Th 4:13 *msihuzunike* kama wanavyofanya watu

HUZUNISHA, Zb 78:41 *wakamhuzunisha* Mtakatifu

Efe 4:30 msiewe *mkiihuzunisha* roho takatifu

HUZUNISHWA, 2Ko 7:9 *mlihuzunishwa* kwa njia ya

IBA, Kut 20:15 *Usiibe*

Met 30:9 *niibe* na kuliaibisha jina la Mungu

Efe 4:28 Mwizi *asiibe* tena

IBADA, Mt 4:10 unapaswa *kumwabudu* Yehova

Yoh 4:24 *wamwabudu* kwa roho na kweli

IBILISI, Mt 25:41 moto wa milele aliotayarishiwa *ibilisi*

Lu 4:6 *ibilisi* akamwambia, nitakupa mamlaka yote

Lu 8:12 *ibilisi* huliondoa neno mioyoni mwao

Yoh 8:44 mmetoka kwa baba yenu *ibilisi*

Efe 4:27 msimpe *ibilisi* nafasi

Efe 6:11 matendo yenye hila ya *ibilisi*

Yak 4:7 mpingeni *ibilisi*, naye atawakimbia

1Pe 5:8 *ibilisi*, anatembea huku na huku

1Yo 3:8 ili avunje kazi za *ibilisi*

Ufu 12:12 Ole kwa sababu *ibilisi* ameshuka kwenu

Ufu 20:10 *ibilisi* atapua ndani ya ziwa la moto

IGA, Ebr 13:7 *igeni* imani yao

IKALIWE, Isa 45:18 aliumba dunia ili *ikalive*

IMANI, Zb 27:13 Ningeukwa wapi [bila] *imani*

Lu 17:6 *imani* inayolingana na mbebu ya haradali

Lu 18:8 atakapofika, kweli ataipata *imani*

Yoh 3:16 kila mtu anayemwamini asiangamizwe

Ro 11:7 mwadilifu ataishi kupitia *imani*

Ro 4:20 alikuwa mwenye nguvu kwa *imani* yake

2Ko 4:13 tunaoonyesha *imani* na kwa hivyo tunasema

2Ko 5:7 tunatembea kwa *imani*, si kwa kuona

Gal 6:10 wale ambao ni ndugu zetu katika *imani*

Efe 4:5 Bwana mmoja, *imani* moja

2Th 3:2 *imani* si mali ya watu wote

2Ti 1:5 ninaikumbuka *imani* yako isiyu na unafiki

Ebr 11:1 *Imani* ni tarajio lililohakikishwa

Ebr 11:6 bila *imani* haiwezekani kumpendeza Mungu

Yak 2:26 *imani* bila matendo imekufa

1Pe 1:7 sifa iliyojaribiwa ya *imani* yenu

IMARA, Yos 1:7 uwe jasiri na imara kabisa

1Ko 1:8 atawafanya ninyi muwe *imara*

1Ko 15:58 iweni *imara*, thabiti

IMARISHWA, Kol 2:7 *kuimarishwa* katika imani

INGILIA, Mdo 5:38 *msingilie* mambo ya watu hawa

ISAKA, Mwa 22:9 Akamfungua *Isaka* mwanawe

ISHARA, Mt 24:3 *ishara* ya kuwapo kwako

Mt 24:30 *ishara* ya Mwana wa binadamu

Lu 21:25 kutakuwa na *ishara* katika jua na mwezi

2Th 2:9 *ishara* za uwongo na mambo ya ajabu

ISHI, Ayu 14:14 Mtu akifa, je, anaweza *kushi* tena?

Ro 14:8 *tukiishi* na tukifa, sisi ni wa Yehova

2Ko 5:15 *wasishi* tena kwa ajili yao wenyewe

ISRAELI, Mwa 35:10 jina lako litakuwa *Israeli*

Zb 135:4 amemchagua *Israeli* awe mali ya pekee

Gal 6:16 amani na rehema, juu ya *Israeli* wa Mungu

ITIA, Ro 10:13 kila mtu anayeliitia jina la Yehova

J

JADILI, Mdo 17:2 *akajadiliana* nao akitumia Maandiko

JALI, Zb 41:1 *anayemjali* mtu wa hali ya chini

Met 14:16 mpumbavu *hajali*, naye anajamini

JANGWA, Isa 35:1 *jangwa* litashangilia na kuchanua

Isa 35:6 vijito katika *jangwa* tamberare

JARIBU, Kum 13:3 Yehova anawajaribu ili ajue

Mal 3:10 nijaribu kwa njia hii

Lu 8:13 wanajaribiwa wanaanguka

Mdo 5:9 milikubaliana kujaribu roho ya Yehova

1Ko 10:9 Wala *tusimjaribu* Yehova

1Ti 3:10 kujaribiwa kama wanafaa

Yak 1:3 sifa iliyojaribiwa ya imani

Yak 1:12 Mwenye furaha anayeyumilia *jaribu*

1Yo 4:1 yajaribu maneno yaliyoongozwa na roho

JASIRI, Yos 1:7 uwe jasiri na imara kabisa

JAZA, Mwa 1:28 mujaze dunia na kuitiisha

JELA, Mdo 5:18 wakawafunga mitume katika *jela*

Mdo 16:26 misingi ya *jela* ikatikiswe

JEMA, Ro 7:19 sifanyi jambo *jema* ninalotaka

JEMBAMBA, Mt 7:13 Ingieni kupita lango *jembamba*

JEMBE, Lu 9:62 anayeshika *jembe* na kutazama nyuma

JENGA, Zb 127:1 Yehova asipojienga nyumba

Isa 65:21 Watajenga nyumba na kuishi ndani yake

Lu 17:28 walikuwa wakipanda, na walikuwa wakijenga

Ro 14:19 tufuatilie mambo yanayoajenga

1Ko 3:10 kila mmoja aangalie jinsi anayoajenga

1Ko 8:1 Ujuzi huleta majiwu, upendo *hujenga*

1Ko 10:23 halali, lakini si yote yanayoajenga

1Ko 14:26 yote na yatendeke kwa ajili ya *kujenga*

Yud 20 *jijenge* juu ya imani yenu takatifu zaidi

JERUHIWA, Ufu 13:3 kichwa chake *kimejeruhiwa*

JESHI, Zb 68:11 Wanawake wanaotangaza ni *jeshi* kubwa

Zek 4:6 Si kwa *jeshi*, bali kwa roho yangu

JIANGALIE, Mdo 20:28 *Jiangelieni* wenyewe na kundi

1Ti 4:16 *Jiangelie* daima na kufundisha kwako

JIBU, Met 15:1 *Jibu* la upole hutuliza hasira

Met 15:23 Mtu hushangilia kutoa *jibu* linalofaa

Met 15:28 mwadilifu hutafakari kabla ya *kujibu*

Met 18:13 anayejibu kabla ya kusikia

Isa 65:24 kabla hawajaita, *nitajibu*

Kol 4:6 mjue *kumjibu* kila mtu

JICHO, Mt 5:38 *Jicho* kwa *jicho* na jino kwa jino

Mt 6:22 Taa ya mwili ni *jicho*

1Ko 2:9 *Jicho* halijaona na sikio halijasikia

1Ko 12:21 *Jicho* haliwazi kuambia mkono, sikuhitaji

1Ko 15:52 kufumba na kufumba *jicho*

JIHADHARI, Met 14:16 Mwenye hekima *jihadhari*

JIJI, Ebr 11:10 *jiji* lililo na misingi ya kweli

JIKWAA, Mt 5:29 jicho lako la kulia linafanya *ujikwae*
JINA, Mwa 11:4 tujijengee *jina* maarufu
 Kut 3:13 nao waniulize, *Jina* lake ni nani?
 Kut 3:15 Yehova, ndilo *jina* langu milele
 Kut 9:16 ili *jina* langu litangazwe duniani
 Kut 20:7 Usilitumie *jina* langu kwa njia isiyofaa
 1Sa 17:45 naja kwa *jina* la Yehova wa majeshi
 1Nya 29:13 kulisifu *jina* lako linalovutia
 Zb 9:10 wanaoijua *jina* lako watakutumaini
 Zb 79:9 Kwa ajili ya *jina* lako tukufu
 Met 18:10 *Jina* la Yehova mnara wenye nguvu
 Met 22:1 afadhali kuchagua *jina* jema kuliko mali
 Mhu 7:1 *Jina* zuri ni bora kuliko mafuta
 Yer 23:27 kufanya watu wangu wasahau *jina* langu
 Eze 39:25 nitalitetea *jina* langu takatifu kwa bidii
 Mal 1:11 *jina* langu litakuwa ku *jina* wataifa
 Mal 3:16 wale wanaolitafakari *jina* lake
 Mt 6:9 *jina* lako na litakaswe
 Yoh 12:28 Baba, litukaze *jina* lako
 Yoh 14:14 Mkiomba lolote katika *jina* langu
 Yoh 17:26 Nimewajulisha *jina* lako
 Mdo 4:12 hakuna *jina* lingine tunaloweza kuokolewa
 Mdo 15:14 mataifa watu kwa ajili ya *jina* lake
 Ro 10:13 anayeliitia *jina* la Yehova ataokolewa
 Flp 2:9 *jina* lililo juu kuliko kila *jina* lingine
JINYENYEKEZENI, Yak 4:10 *Jinyenyekezeni* machoni pa
 1Pe 5:6 *jinyenyekezeni* chini ya mkono wa Mungu
JIPYA, Mdo 17:21 kuambiana au kusikiliza jambo *jipya*
JIRANI, Lu 10:27 mpende *irani* unavyojipenda
 Lu 10:36 ni nani aliyekuwa *irani* ya mtu huyo?
JITAHIDI, Lu 13:24 *Jitahidini* sana ili mwingie kupitia
JITHADINI, 2Pe 1:5 *Jitahidini* kuongeza kwenye imani
JITISHENI, 1Pe 2:13 *Jitisheni* yenyewe kwa mfalme
JIVUNA, 2Th 1:4 *tunajivuna* ninyi kati ya makutaniko
JIWE, Da 2:34 *jiwe* likakatawa, si kwa mikono
 Mt 21:42 *Jiwe* ambalo wajenzi walilikataa
JIWE LA PEMBENI, Zb 118:22 *jiwe kuu la pembeni*
 Efe 2:20 Yesu ndiye *jiwe* la msingi *la pembeni*
JOGOO, Mt 26:34 kabla *jogoo* hajawika, utanikana
JOKA, Ufu 12:9 *joka* mkubwa akatupanua chini
JUA, Yos 10:12 *Jua*, simama tuli juu ya Gibeoni
 Mt 24:29 baada ya dhiki huyo *jua* litatiwa giza
 Mdo 2:20 *Jua* litatiwa giza
JUMA, 1Ko 16:2 Siku ya kwana ya *juma*, weka kando

K

KAACHO, 1Ko 16:13 *Kaeni macho*, simameni imara
 Ufu 16:15 Mwenye furaha ni yule anayekaa *macho*
KABIDHI, Lu 16:11 nani atawakabidhi kilicho ka kweli?
 1Pe 2:23 *alijkabidhi* mkononi mwa Yule anayehukumu
 1Pe 4:19 *ujikabidhi* wenyewe kwa Muumba mwaminifu
KABILI, Flp 1:23 *Ninakabiliwa* na mambo haya mawili
KABURI, Ayu 14:13 Laiti ungenificha *Kaburini*
 Mhu 9:10 hakuna kazi wala hekima *Kaburini*
 Ro 13:14 Nitawakomboa kutoka katika *Kaburi*
 Yoh 5:28 wote walio katika *makaburi* wataisikia sauti
 Mdo 2:31 Kristo hakuchwa katika *Kaburi*
 Ufu 1:18 nina funguo za kifo na za *Kaburi*
 Ufu 20:13 kifo na *Kaburi* vikawatoa wafu
KAHABA, Met 7:10 amevaa kama *kahaba*
 1Ko 6:16 ameingana na *kahaba* ni mwili mmoja
 Ufu 17:1 *kahaba* anayekaa juu ya maji mengi
 Ufu 17:16 watamchukua yule *kahaba* na kumfanya
KAINI, 1Yo 3:12 si kama *Kaini* aliyemua ndugu yake
KAISARI, Mt 22:17 kumlipa *Kaisari* kodi
 Mk 12:17 Miipeni *Kaisari* vitu vya *Kaisari*
 Yoh 19:12 Ukimfungua, wewe si rafiki ya *Kaisari*
 Yoh 19:15 Sisi hatuna mfalme ila *Kaisari*
 Mdo 25:11 Ninakata rufaa kwa *Kaisari*
KALEBU, Hes 13:30 *Kalebu* akajaribu kuwatuliza watu
 Hes 14:24 *Kalebu* alikuwa na roho tofauti
KALI, Met 15:1 neno *kali* huchochea hasira
KAMBA, Mhu 4:12 *kamba* ya nyuzi tatu haikatiki upesi
 Isa 54:2 refusha *kamba* za hema lako
KAMILI, 1Nya 28:9 kumtumikia kwa moyo *kamili*
 2Nya 16:9 wale ambao moyo wao ni *kamili*
 1Ko 13:9 tuna ujuzi usio *kamili*

KAMILIFU, Kum 32:4 Mwamba, kazi zake ni *kamilifu*
 Zb 19:7 Sheria ya Yehova ni *kamilifu*
KANA, Kut 30:9 nisishibe na *kukukana*
 Mt 16:24 lazima *ajikane* mwenyewe
 Mk 14:30 *utunikana* mara tatu
 Yoh 2:1 karamu ya ndoa katika *Kana*
 Mdo 26:11 nikajaribu kuwalazimisha *wakane* imani
 Tit 1:16 *wanamkana* kwa matendo yao
KANDAMIZA, Mhu 4:1 *waliowakandamiza* wana nguvu
KANYAGA, Ebr 10:29 *amemkanyagia* chini Mwana wa
KARAMU, Isa 25:6 *Karamu* ya vyakula vinono
 Ro 13:13 si katika *karamu* zenye vurugu
 Gal 5:21 uelevi, *karamu* zenye vurugu
KARIBIA, Zb 73:28 *kumkaribia* Mungu ni jambo jema
 Yak 4:8 *Mkaribieni* Mungu, naye atawakaribia
KARIBISHA, Ro 12:13 Iweni *wakaribishaji* wageni
 Tit 1:7, 8 Mwangalizi awe *mkaribishaji* wageni
 Ebr 13:2 Msisahau *kuwakaribisha* wageni
 1Pe 4:9 *Mkaribishane* bila kunung'unika
 3Yo 8 wajibu wa *kuwakaribisha* watu hao
KARIBISHANA, Ro 14:1 *Mkaribisheni* mwenye udhaifu
 Ro 15:7 *mkaribishane*, kama vile Kristo
KARIBU, Zb 145:18 Yehova, *karibu* na wanaomwitia
KARIPIA, Zb 141:5 *Akinakaria*, litakuwa kama mafuta
KARIOPIO, Met 3:11 usichukie *karipio* lake
 Met 27:5 *Karipio* la wazi ni afadhali kuliko
 Mhu 7:5 afadhali kusikiliza *karipio*
KARIPIWA, Met 29:1 shingo ngumu baada ya *kukaripwiwa*
KASIRIKA, Zb 37:8 *Usikasirike* na kuanza kutenda uovu
 Met 21:19 mke mgomvi anayekasirika haraka
 Efe 4:26 jua lisitue mkiwa *nmekasirika*
KASIRISHA, Efe 6:4 msiwe *mkwakasirisha* watoto wenu
 Kol 3:21 akina baba, msiwe *mkwakasirisha*
KASORO, Law 22:21 hapaswi kuuwa na *kasoro* yoyote
KATAA, Yer 8:9 *Wamelikataa* neno la Yehova
KATALIWA, 1Ko 9:27 mimi mwenyewe nisikataliwa
KATA TAMAA, Ro 5:5 tumaini *halikatisi tamaa*
 Ro 9:33 yeye anayemwamini hatakata tamaa
KATAZA, Mdo 5:28 *Tuliwakataza* msifundishe
KATILIWA MBALI, Mt 25:46 watakatiliwa mbali milele
KAULI MOJA, Mdo 15:25 tumefikia *kauli moja*
KAWAIDA, Mdo 4:13 wasio na elimu na wa *kawaida* tu
KAWIA, Isa 46:13 wokovu wangu *hautakawia*
 Hab 2:3 Hata *yakikawia*, endelea kuyatarajia!
 Lu 12:45 Bwana wangu anawakia juu
 2Pe 3:9 Yehova *hakawii* kuhusu ahadi yake
KAZA, Kol 3:2 Edeleeni *kukaza* akili zenu kwenye
KAZI, Ne 4:6 wakafanya kazi kwa moyo wote
 Zb 104:24 Jinsi kazi zako zilivyo nyingi
 Mhu 2:24 kufurahia kazi yake ngumu
 Yoh 5:17 Baba anaendelea kufanya kazi
 Yoh 6:27 Msifanyie kazi chakula kinachoharibika
 Yoh 14:12 atafanya kazi kubwa kuliko hizi
 Efe 4:28 asiibe tena; afanye kazi kwa bidii
 1Th 2:9 Tulifanya kazi usiku na mchana
 2Th 3:10 asiyetaka kufanya kazi, asile chakula
KEFA, 1Ko 15:5 alimtokea Kefa, kisha wale 12
 Gal 2:11 Kefa alipokuja Antiokia, nilimpinga
KENGESHWA, Lu 10:40 Martha *alikengeshwa* na kazi
 1Ko 7:35 kumtumikia Bwana bila *kukengeshwa*
KERUBI, Eze 28:14 Nilikuweka kuwa *kerubi* anayefunika
KESHA, Mt 26:41 Edeleeni *kukeshwa* na kusali
 Lu 21:36 edeleeni *kukeshwa* mkiomba dua
KESHO, Met 27:1 Usijijamba kuhusu *kesho*
 1Ko 15:32 tute na tunywe, *kesho* tutakufa
KETI, Zb 110:1 Keti kwenye mkono wangu wa kuume
KIANGAZI, Mt 24:32 mnajua *kiangazi* kinakaribia
KIASI, Met 11:2 wenye *kiasi* wana hekima
 Mik 6:8 utembeke kwa *kiasi* na Mungu wakol
 1Ti 2:9 wanawake kujipamba kwa *kiasi*
KIBALI, Isa 26:10 Hata mwovu akionyesha *kibali*
 1Ko 7:33 kupata *kibali* cha mke
KIBURI, Met 8:13 Ninachukua kujikweza na *kiburi*
 Met 16:5 mwenye *kiburi* moyoni humchukiza Yehova
 Met 16:18 *Kiburi* hutangulia kuanguka
KICHAKA, Mdo 7:30 akamotokea katika *kichaka*
KICHEKO, Mt 14:13 katika *kicheko* moyo wana maumivu

KICHWA, Mwa 3:15 atakuponda *kichwa*
 Da 2:32 *Kichwa* cha sanamu kilikuwa dhahabu
 1Ko 11:3 *kichwa* cha mwanamke ni mwanamume
 Efe 5:23 Kristo *kichwa* cha kutaniko
 Efe 5:23 mume ni *kichwa* cha mke wake

KIDOLE, Kut 8:19 Ni *kidole* cha Mungu!
 Kut 3:18 mabamba yaliyoandikwa kwa *kidole*

KIELELEZO, Yoh 13:15 nimeweawekea *kielelezo*
 1Ko 10:6 mambo hayo yalikuwa *vielelezo* kwetu
 Ebr 8:5 tengeneza vitu vyote kwa kufuata *kielelezo*
 1Pe 2:21 Kristo aliwaachia ninyi *kielelezo*
 1Pe 5:3 kuwa *vielelezo* kwa kundi

KIFAA, Mhu 10:10 *kifaa* cha chuma hakina makali
KIFAPA, Mt 4:24 wenye *kifapa*, waliopooza, akawaponya
KIFO, Ru 1:17 tutenganisha isipokuwa *kifo*
 Zb 89:48 mwanadamu gani asiyezuwa kuona *kifo*?
 Isa 25:8 Atameza *kifo* milele
 Eze 18:32 sifurahii *kifo* cha mtu yeyote
 Ho 13:14 *Kifo*, yako wapi maumivu yako?
 Yoh 8:51 akishika maneno yangu, hataona *kifo*
 Ro 5:12 *kifo* kikaenea kwa watu wote
 Ro 6:23 mshahara ambao dhambi hulipa ni *kifo*
 1Ko 15:26 adui wa mwisho atakayeangamizwa ni *kifo*
 1Th 4:13 wale wanaolala usizingi katika *kifo*
 Ebr 2:9 aonje *kifo* kwa ajili ya kila mtu
 Ebr 2:15 watumwa kwa sababu ya kuogopa *kifo*
 Ufu 21:4 *kifo* hakitakuwapa tena

KIFO CHA PILI, Ufu 2:11 *kifo* cha *pili* hakitamduru
 Ufu 20:6 *kifo* cha *pili* hakina mamlaka juu ya hao
 Ufu 20:14 *kifo* cha *pili*, ile ziwa la moto

KIFUA, Isa 40:11 atawabeba kwenye *kifua* chake
KIFUNGO, Efe 4:3 *kifungo* cha muungano cha amani
 Kol 3:14 upendo, *kifungo* kikamilifu cha muungano
KIGEZO, 2Ti 1:13 *kigezo* cha maneno yenye manufaa
KIINITETE, Zb 139:16 ulionina nikiwa *kiinitete*
KIJANA, Ayu 33:25 Mwili wenye afa kuliko wa *ujana*
 Zb 71:17 umenifundisha tangu nikwa *kijana*
 Mk 10:20 nimeyashika tangu nilipokuwa *kijana*
KIJIA, Met 4:18 *kijia* cha waadilifu ni kama nuru
KIKOMBE, Mt 20:22 mnaeweza kunywa *kikombe*
 Lu 22:20 *Kikombe* hiki kinamaanisha agano jipya
 Lu 22:42 ukipenda, niondolea *kikombe* hiki
 1Ko 11:25 Akafanya vivyo hivyo na kile *kikombe*

KIKWAZO, Ro 14:13 kutoweke *kikwazo*

KILEMA, Isa 35:6 *kilema* ataruka kama paa
 Mal 1:8 mnapomtoa mnyama *kilema* au mgonjwa
KILEMBA, Eze 21:26 Kiondo *kilemba*, na ulivue taji
KILEO, Met 20:1 Divai ni mdhihaki, *kileo* ni vurugu
KILIO, Isa 35:10 huzuni na *kilio* vitatoweke
KIMAKUSUDI, Ebr 10:26 kutitenda dhambi *kimakusudi*
KIMBELEMBELE, Kum 17:12 *kimbelembele* kwa kutosikiliza
 1Sa 15:23 kutenda kwa *kimbelembele* ni sawa na
 Zb 19:13 unizue nisitende kwa *kimbelembele*
 Met 11:2 *Kimbelembele* kikijia, aibu itafuata
KIMBIA, 1Ko 6:18 *Ukimbieni* usherati!
 1Ko 9:24 wakimbaji *hukumbia* ili kushinda
 Gal 5:7 Mlikuwa *mnaakimbia* vema. Nani
KIMBILIO, Zb 9:9 Yehova *kimbilio* salama
 Sef 3:12 watapata *kimbilio* katika jina la Yehova
KIMWILI, 1Ko 2:14 mtu wa *kimwili* hayakubali
 1Ko 3:3 bado ninyi ni wa *kimwili*
 Kol 2:18 kwa akili yake ya *kimwili*

KIMYA, Isa 53:7 kondoo aliye *kimya* mbele ya
KINA, Ro 11:33 Jinsi kilivyo *kina* cha utajiri wa Mungu
 1Ko 2:10 roho, mambo yenye *kina*
 Efe 3:18 kufahamu kikamilii *kina*

KINABILI, 2Pe 1:19 neno la *kinabili* limefanywa hakika zaidi
KINYESI, Kum 23:13 kuchimba shimo na kufunika *kinyesi*
KINYONGO, Law 19:18 usiwe na *kinyongo* dhidi ya
KINYWA, Kum 25:4 usimfungue *kinywa* ng'ombe
 Zb 8:2 Kutoka katika *vinywa* vya watoto
 Lu 6:45 *kinywa* husema yaliyojaa moyoni
 Ro 10:10 kwa *kinywa* hufanya tangazo la hadharani
 Yak 3:10 Baraka na laana *kinywa* kilekile

KIONGOZI, Met 28:16 *Kiongozi* anayetumia mamlaka
 Mt 23:10 *Kiongozi* wenu ni mmoja, Kristo
KIOO, 1Ko 13:12 kupitia *kioo* cha chuma
 Yak 1:23 anayetazama uso wake katika *kioo*

KIPIMO, Lu 6:38 kwa *kipimo* mnachowapimia watu
KIPOFU, Law 19:14 usiweke kizuizi mbele ya *kipofu*
 Isa 35:5 macho ya *kipofu* yatafunguliwa
 Mt 15:14 Wao ni viongozi *vipofu*

KIROHO, Mt 5:3 wanaotambua uhitaji wao wa *kiroho*
 Ro 1:11 niwape zawadi ya *kiroho*
 1Ko 2:15 mtu wa *kiroho* huchunguza mambo yote

KISASI, Kum 32:35 *Kisasi* ni changu, na malipo
 2Th 1:8 atakaopeta *kisasi* juu ya wale

KISIKI, Isa 11:1 tawi kwenye *kisiki* cha Yese
 Da 4:15 kiacheni *kisiki* na mizizi yake

KISINGIZIO, Yoh 15:22 hawana *kisingizio* cha dhambi
 Yud 4 *kisingizio* cha mwenendo mpotovu

KITABU, Kut 32:33 nitamfuta katika *kitabu* changu
 Yos 1:8 *Kitabu* hiki cha Sheria kisiondoke
 Mal 3:16 *kitabu* cha kumbukumbu kikaandikwa
 Ufu 20:15 kundiwa katika kile *kitabu* cha uzima

KITAMBA, 2Ko 3:15 *kitamba* hukaa juu ya miyojo yao
KITANDA, Zb 41:3 atamtegemea kwenye *kitanda* chake
 Ebr 13:4 *kitanda* cha ndoa kisiwe na unajisi

KITI CHA HUKUMU, Yoh 19:13 Pilato, *kiti* cha *hukumu*
 Ro 14:10 mbele ya *kiti* cha *hukumu* cha Mungu

KITI CHA UFALME, Zb 45:6 Mungu ni *kiti* cha *ufalme*
 Isa 6:1 Yehova ameketi, *kiti* cha *ufalme*
 Mt 25:31 Mwana wa binadamu ataketi, *kiti* cha *ufalme*
 Lu 1:32 Mungu atampa *kiti* cha *ufalme* cha Daudi

KITU, Gal 6:3 akifikiri yeye ni *kitu* wakati yeye si *kitu*
KITU KISICHOFAA, Zb 101:3 sitaweka *kitu kisichofaa*
KITULIZO, 2Th 1:7 mnaopata dhiki mtpata *kitulizo*
KIU, Isa 49:10 hawatakuwa na *kiu*
 Isa 55:1 Njooi, nyote mlio na *kiu*
 Yoh 7:37 aliye na *kiu*, na aje

KIUNGO, 1Ko 12:18 Mungu amepanga kila *kiungo*
KIVULI, 1Inya 29:15 siku zetu ni kama *kivuli*
 Zb 91:1 Ataishi katika *kivuli* cha Mweza-Yote
 Kol 2:17 Mambo hayo ni *kivuli*
 Yak 1:17 habadiliki kama *kivuli*

KIWANGO, Yeh 30:11 nidhamu kwa *kiwango* kinachofaa
KIZAZI, Mt 24:34 *kizazi* hiki hakitapitia mbali
KIZIWI, Law 19:14 Usimtukane *kiziwi*
 Isa 35:5 masikio ya *viziwi* yatazibulwa
 Mk 7:37 anafanya *viziwi* wasikie

KODI, Mt 17:25 Wafalme hupokea *kodi* kwa nani
 Lu 20:22 ni halali kumpia Kaisari *kodi*?
 Lu 23:2 kukataza wasimlie Kaisari *kodi*
 Ro 13:6 Ndiyo maana mnalipa *kodi*
 Ro 13:7 anayetaka *kodi*, *kodi*

KOFI, Yoh 19:3 walikuwa wakimpiga *makofi* usoni
KOFIA, Efe 6:17 pokeeni *kofia* ya chuma ya wokovu
KOMAA, Efe 4:13 kuwa mtu *aliyekomaa* kabisa
KOMBOA, Zb 49:7 anayeweza *kumkomboa* ndugu
 Ho 13:14 *Nitawakomboa* kutoka katika Kaburi
 2Pe 2:9 Yehova anajua *kuwakomboa* watu

KONDOO, Zb 100:3 watu wake na *kondoo* wa malisho
 Isa 53:7 Aliletwa kama *kondoo* machinjoni
 Eze 34:12 Nitawatunza *kondoo* wangu
 Mt 25:33 atawaweke *kondoo* kuume
 Yoh 21:16 Chunga *kondoo* wangu wadogo
KONDOO WENGINE, Yoh 10:16 nina *kondoo wengine*
KOPESHA, Met 19:17 *anamopesha* Yehova
 Lu 6:35 *kukopesha* bila kutamaini kurudishwa

KORA, Hes 26:11 wana wa Kora hawakufa
 Yud 11 maneno ya uasi ya Kora

KORESHI, Eze 6:3 *Koreshi*: Nyumba hiyo na ijenge upya
 Isa 45:1 mtiwa-mafuta wake, *Koreshi*

KORNELIO, Mdo 10:24 *Kornelio* aliwakusanya watu wake
KOSA, Ayu 6:24 Nisaidieni kuelewa *kosa* langu
 Zb 40:12 *Makosa* yangu ni mengi kuliko nywele
 Zb 130:3 Ikiwa ungukuwa unatazama tu *makosa*
 Isa 53:5 alichomwa kwa sababu ya *makosa* yetu
KOSOA, 1Ti 5:1 *Usimkosoe* mwanamume mzee

KRISTO, Mt 16:16 Wewe ndiye *Kristo*, Mwana wa
 Lu 24:26 haiukuwa lazima *Kristo* kupatwa na mateso?
 Yoh 17:3 na yule yuliyemta, Yesu *Kristo*
 Mdo 18:28 kwa Maandiko kuwa Yesu ndiye *Kristo*
 1Ko 11:3 *kichwa* cha *Kristo* ni Mungu
KRISTO WA UWONGO, Mt 24:24 *Kristo* wa uwongo

KUACHA, Kum 31:8 Hatakutupa wala *kukuacha*
 1Sa 12:22 Yehova *hatawaacha* wata wake
 Zb 27:10 Hata baba na mama *wakiniacha*
 Zb 37:28 Yehova *hatawaacha* washikamanifu
 Yoh 8:29 *hakuniacha*, kwa sababu sikuzote
 Mdo 5:42 kufundisha na kutangaza bila *kuacha*
 Ebr 13:5 Sitakuacha wala kukutupa kamwe

KUBALI, Ayu 2:10 Je, *tukubali* tu mema kutoka
 Lu 3:22 Mwanangu, mpenda; *nimekukubali*
 2Ti 2:15 ujitoe kwa Mungu ukiwa mtu *aliyekubaliwa*
KUBALIKA, 2Ko 6:2 Sasa ndio wakati *anaokubalika*
 Efe 5:10 kuhakikisha *linalokubalika* kwa Bwana

KUBOMOA, Ro 14:20 Acheni *kuibomoa* kazi ya Mungu
 KUBWA, Ro 13:1 ajititshie kwa mamlaka zilizo *kubwa*
KUCHANGANYA, 2Ko 4:2 *kulichanganya* neno la Mungu
KUCHANUA, Isa 35:1 jangwa tamberare *litachanua*
KUCHINJAWA, Zb 44:22 kondoo wa *kuchinjwa*
KUCHOCHEANA, Ebr 10:24 *kuchocheana* katika upendo
KUCHUKIZA, Mt 24:15 kitu chenye *kuchukiza*
KUELEZA, Mdo 17:3 *akieleza* na kutibitisha kwa marejejo
KUFA, Mwa 3:4 Hakika *hamtakufa*
 Ayu 14:14 Mtu *akifa*, je, anaweza kuishi tena?
 Mhu 9:5 *waliokufa* hawajui lolote kamwe
 Lu 15:24 mwanangu alikuwa *amekufa*
 Lu 20:38 si Mungu wa wafu, bali walio hai
 Yoh 11:25 hata *akifa*, ataishi tena
 Yoh 11:26 anayemiambi hatakuwa kamwe
 Ro 14:8 tukifa, *tuakufa* kwa ajili ya Yehova
 1Ko 15:53 huu unaoweza *kufa* uvae kutoweza *kufa*
 2Ko 5:15 yule *aliyekufa* kwa ajili yau na kufufuliwa
 Efe 2:1 hai, ingawa mlikuwa wafu
 1Th 4:16 *waliokufa* katika muungano na Kristo
 Ufu 14:13 *wanaokufa* katika muungano na Bwana

KUFAA, 1Ko 11:27 kunywa kikombe *isivyofaa*
 Ebr 11:38 ulimwengu *haukuwafaa*

KUFA GANZI, Zb 143:4 Moyo wangu *umekufa ganzi*
KUFA MOYO, 2Ko 4:1 tuna huduma hii *hatufi moyo*
 2Ko 4:16 hatufi moyo, lakini hata ikiwa mtu
 Gal 6:9 *tusife moyo* kufanya mema

KUFIKIRI, Met 12:18 Maneno yanayosema bila *kufikiri*
 Met 19:2 anayetenda bila *kufikiri* anenda dhambi
 Met 29:20 umemwona mtu anayongoa bila *kufikiri?*

KUFOKA, Efe 4:31 hasira, ghadhabu, *kufoka*
KUFUNGA, Isa 58:6 *kufunga* ambako ninachagua
 Lu 18:12 Mimi *hufunga* mara mbili kwa juma

KUFURU, Mk 3:29 *anayekufuru* roho takatifu
KUGEUKA SURU, Mt 17:2 *Suru* yake *ikeguka* mbele yao
KUGEUZWA, Ro 12:2 *mgeuzwa* kwa kufanya upya akili
KUHANI, Zb 110:4 *kuhani* milele, Melkizedeki
 Ho 4:6 ujuzi, nitawakataa msiwe *mukahani*
 Mal 2:7 midomo ya *kuhani* inapaswa kulinda ujuzi
 Ebr 2:17 *kuhani* mkuu mwenye rehema na mwaminifu

KUHARIBIKA, 1Ko 15:42 hufufuliwa katika *kutoharibika*
KUHUBIRI, Mt 9:35 Yesu *akahubiri* habari njema
 Lu 8:1 *akihubiri* na kutangaza habari njema

KUIMBA, Mt 26:30 baada ya *kuimba* sifa, waikaenda
 Efe 5:19 *mkiimba* na kupiga muziki
 KUJA, Mdo 1:11 *atakuja* kama alivyoeenda angani
KUJARIBU, 2Ko 13:5 *kujjaribu* kama mko katika imani
KUJAMINI, Met 14:16 mpumbavu *anjamani* kupita
KUJIFUNZA, Kum 4:10 Wakusanye ili *wajifunze*
 Flp 4:9 Mambo *mliyojifunza* na vilevile
 2Ti 3:7 *wakijifunza* sikuzote lakini hawawezi

KUJIINGIZA, 1Ti 5:13 *kujjiingiza* katika mamba ya watu
 1Pe 4:15 *kujjiingiza* katika mamba

KUJKATA, Law 21:5 Hawapaswi *kujikatakata*
KUJKIWA, Yak 3:2 sote *hujikiwa* mara nyingi
KUJIONYESHA, 1Yo 2:16 *kujionyesha* mali zake maishani
KUJIPA MOYO, Mdo 28:15 Paulo *akajipa moyo*
KUJISIFU, 1Ko 1:31 anayesifua, na *ajisifu* katika Yehova
 Flp 2:3 Msifanye jambo lolote kwa *kujisifu*

KUJITENGA, Met 18:1 *anayejitenga* anafuatia
KUJITETEA, Ro 1:20 hawana sababu ya *kujitetea*
 1Pe 3:15 mkiwa tayari *kujitetea*

KUJITIISHA, Ro 13:1 *ajititshie* kwa mamlaka kubwa
KUJITOLEA, Kut 36:2 moyo wake ulimsukuma *kujitolea*
KUJIZIWA, 1Ko 7:5 kuwaribu kwa kukosa *kujizuia*
 Gal 5:22, 23 tunda la roho ni *kujizuia*
 2Ti 2:24 *anayejizuia* anapokosewa

KUJUA, Yer 31:34 *Mjue* Yehova! wote watanijua
 Gal 4:9 sasa Mungu *amewajua* ninyi

KUJUA MIMI NI YEHOVA, Kut 7:5 watajua *mimi ni Yehova*
 Eze 39:7 mataifa *yatajua mimi ni Yehova*

KUKAZIA, Kum 6:7 lazima *uyakazie* kwa wanao
KUKESHA, 1Pe 4:7 *kukेशa* kuhusiana na sala
KUKOSA USINGIZI, 2Ko 6:5 kwa *kukosa usingizi* usiku
 2Ko 11:27 mara nyingi *kudhosa usingizi* usiku
KUKOSEWA, 1Ko 6:7 si afadhali mkubali *kukosewa*
KUKU, Mt 23:37 *kuku* anavyokusua vifaranga
KUKUTANA, Ebr 10:25 bila *kuacha kukutana* pamoja
KUKWAZA, Mt 13:41 vitu vinavyosababisha *kukwazika*
KULA, 1Ko 5:11 hata *msile* chakula pamoja naye
KULALA, 1Th 5:6 tusiendelee *kulala* kama wengine
KULIA, Isa 65:19 sauti ya *kulia* hataisikika tena
 Ho 12:4 *Allia* na kumsihi apate kibali
 Mt 26:75 Petro akaenda *nie akalia* kwa uchungu
 Lu 6:21 Wenye furaha ni ninyi *mnaolia*
 Ro 12:15 *lieni* na wale *wanaolia*

KUMBUKA, Ayu 14:13 ongepima wakati na *kunikumbuka*
 Mhu 12:1 *mkumbuka* Muumba kwa Mkuu
 Lu 12:19 Endeeleni kufanya hivi *kunikumbuka*
 Ebr 10:32 endeeleni *kuzikumbuka* siku za zamani

KUMBUSHA, 2Pe 1:12 ninakusudia *kuwakumbusha* haya
KUMI, Mwa 18:32 Sitaliangamiza kwa ajili ya hao *kumi*
KUMSTAHILI, Kol 1:10 *kumstahili* Yehova
KUMWOGOPA YEHOVA, Zb 19:9 *Kumwogopa Yehova* ni
 Zb 11:10 *Kumwogopa Yehova* ni mwanzo wa hekima
 Met 8:13 *Kumwogopa Yehova*, kuchukia uovu

KUNDI, Lu 12:32 Msiogope, ninyi *kundi* dogo
KUNDI DOGO, Lu 12:32 Msiogope, ninyi *kundi dogo*
KUNGOJEA, Mik 7:7 mtazamo wa *kumngojea*
KUNI, Met 26:20 Pasipo na *kuni* moto huzimika
KUNUNG'UNIKA, Flp 2:14 mamba, bila *kunung'unika*
KUOGOPA, Met 29:25 *Kuwaogopa* wanadamu ni mtego
KUONYA, Eze 33:9 *ukimwonya* mwovu aiache njia yake
KUPAMBA, Tit 2:10 *walipamba* fundisho la Mungu
KURA, Zb 22:18 wanalipigia *kura* vazi langu
 Lu 23:51 Mtu huyo hakupigia *kura* kungu mkono
KUREKEBISHA, 2Ko 13:11 *kurekebisha* upya, kufarijiwa
 Gal 6:1 *kmurekebisha* kwa roho ya upole
 Efe 4:12 *kuwarekebisha* watakatifu

KURIDHIKA, Flp 4:11 nimejifunza *kuridhika*
KUSANYA, Efe 1:10 *kukasanya* vitu vyote katika Kristo
KUSHINDA, Ro 8:37 tunatoka tukiwa *tumeshinda* kabisa
KUSTAAJABISHA, Zb 139:14 kwa njia ya *kustaajabisha*
KUSTAHILI, Mt 10:37 kuliko anavyonipenda *hanistahili*
 Lu 15:19 *Sistahili* tena kuitwa mwanao
 Mdo 5:41 *wamestahili* kuvunjiwa heshima
 Mdo 13:46 kujiona *hamstahili* uzima wa milele
 2Th 1:5 kuhesabiwa kuwa *mnanstahili* Ufalme wa Mungu

KUSUBIRI, Ro 8:25 *kukisubiri* kwa hamu na uvumilivu
KUSUDI, Met 16:4 amefanya kila kitu kimitize *kusudi* lake
 Ro 8:28 wameitwa kulingana na *kusudi* lake
 Ro 9:11 *kusudi* la Mungu halitegemei matendo
 Efe 3:11 kulingana na *kusudi* la milele

KUTAFUTA, Mhu 7:25 *kutafuta* hekima na maana
KUTANIKO, Zb 22:25 Nitakusifua katika *kutaniko* kubwa
 Zb 40:9 Kutangaza habari njema katika *kutaniko* kubwa
 Mt 16:18 juu ya mwamba huu nitajenga *kutaniko* langu
 Mdo 20:28 milichunge *kutaniko* la Mungu
 Ro 16:5 salimuni *kutaniko* lililo katika nyumba yao

KUTEMBEA, Mik 6:8 *utembea* kwa kiasi na Mungu wako
 Yoh 6:19 wakamwona Yesu *akitembea* juu ya bahari
KUTENGANA, 1Ko 7:10 hapaswi *kutengana* na mume
KUTHIBITISHA, Mdo 17:3 akieleza na *kuthibitisha* kwa
KUTIA MOYO, Mdo 13:15 neno la *kuwatia moyo*, litemeni
 Mdo 14:22 *kuwatia moyo* wabaki katika
 Ro 1:12 badala yake, *tutiane moyo*
 Tit 1:9 *kuta moyo* kwa fundisho na kukaripia
KUTIANA MOYO, Ro 1:12 badala yake, *tutiane moyo*
 Kol 3:16 Endeeleni *kutiana moyo*
 Ebr 10:25 *tutiane moyo*, na kufanya hivyo zaidi

KUTIA NGUVU, 1Sa 30:6 *akajitia nguvu* kwa msaada wa
 Isa 35:3 *itiene nguvu* mikonu iliyo dhafu
 Lu 22:32 *watie nguvu* ndiguo zako
KUTII, Lu 2:51 akaendele *kuwatie*
KUTOA, Mdo 20:35 furaha katika kutoa kuliko kupokea

KUTOJALI, Met 1:32 *kutojali* kwa wapumbavu
KUTUMIA VIBAYA, 1Ko 9:18 *nisitumie vibaya* mamlaka
KUTUMIWA, 2Ko 12:15 *kutumwiwa* kabisa kwa ajili yenu
KUUGUA, Ro 8:22 uumbaji wote unaelekea *kuugua*
 Ro 8:26 roho hutumboa kwa *kuugua* kusikotamkwa
KUWA, Kut 3:14 *Nitakuwa* Kile Ninachochagua *Kuwa*
 1Ko 9:22 *Nimekuwa* mambo yote kwa
KUWAPA, Mt 24:3 nini ishara ya *kuwapa* kwako?
 Mt 24:37 kama siku za Noa, ndivyo *kuwapa* kwa
 2Pe 3:4 Kuko wapi huko *kuwapa* kwake
KUWASILIANA NA ROHO, Gal 5:20 *kuwasiliana* na roho
KUZUIA, 1Th 2:16 *kutuziua* kuzungumza na watu
KWA KUSTAHILI, Efe 4:1 mtembele kwa *kustahili* mwito
KWA NDANI, Ro 7:22 mtu niliye *kwa ndani*
KWANZA, Mt 19:30 wa *kwanza* watakuwa wa mwisho
 Mk 9:35 anayetaka kuwa wa *kwanza*, lazima
KWAZA, Zb 119:165 sheria, hakuna cha *kuwakwaza*
 Lu 17:2 kuliko *amkwaze* mmoja wa hawa
 1Ko 8:13 chakula *kinamkwaza* ndugu yangu
 Flp 1:10 msiwé *mkwakwaza* wengine
KWELI, Zb 119:160 Kiini cha neno lakini ni *kweli*
 Met 23:23 Inunue *kweli* wala usiue
 Yoh 4:24 wamwabudu kwa roho na *kweli*
 Yoh 8:32 mtajua *kweli*, nayo *kweli* itawakehwa huro
 Yoh 14:6 Mimi ndiye njia na *kweli* na uzima
 Yoh 16:13 roho ya *kweli*, atawaongoza kwenye *kweli*
 Yoh 17:3 wakujue, Mungu wa pekee wa *kweli*
 Yoh 17:17 neno lako ni *kweli*
 Yoh 18:38 Pilato akamuuliza: *Kweli* ni nini?
 2Ko 13:8 kufanya lolote kinyume kwa *kweli*
 1Ti 6:19 waushike uzima ulio wa *kweli*
 2Pe 1:12 mko imara katika *kweli*
 3Yo 4 watoto wangu wanatembea katika *kweli*

L

LAANA, Hes 23:8 Ninawezaje *kuwalaani* watu ambao
 Yoh 7:49 umati huu ni watu waliolaaaniwa
 Ro 12:14 muwe mkibariki msiwe *mkilaani*
LAGHAI, Law 19:13 *Usimlaghai* mwenzako
LAINI, Met 25:15 ulimi *laini* unaweza kuvunja mfupa
 Ro 16:18 hushawishi kwa maneno *laini*
LALA, Met 6:10 *Lala* kidogo, sinzia kidogo
LANGO, Mt 7:13 Ingingi kupitia *lango* jembamba
LAWI, Mal 3:3 atawakasha wana wa *Lawi*
LAZARO, Lu 16:20 akiombaomba aliyetwa *Lazaro*
 Yoh 11:11 *Lazaro* amela usingizi
 Yoh 11:43 *Lazaro*, njoo huko njie!
LAZIMA, Ro 12:3 asijifikirie kuliko iliyo *lazima* kufikiri
LEMAZWA, Isa 44:8 *msilemzwa* na woga
LEMEA, Zb 40:12 Makosa yangu *yanilemea*
LEMEWA, Lu 21:34 miyo yenu isilemewe kamwe
LEWA, Efe 5:18 *msilewe* dawai
LIA, Eze 9:4 watie alama *wanaolia*
LIDIA, Mdo 16:14 *Lidia*, muuzaji wa nguo za zambarau
LINDA, Met 4:23 *Ulinde* moyo wako kuliko vitu vyote
LINGANISHA, Isa 46:5 *kunilinganisha* na nani
 Gal 6:4 si kwa *kujilinganisha* na mtu mwingine
LIPA, Kut 21:36 lazima alipe
 Zb 37:21 Mwovu hukopa lakini *halipi*
 Zb 116:12 *Nitamlipa* Yehova nini
 Ro 12:19 Kisasi ni changu; mimi *nitalipa*
 2Th 1:6 *kuwalipa* dhiki wanaowasababishia
LIPA KISASI, Ro 12:19 Wapendwa, *msijilipizie kisasi*
LIPIZA, Met 20:22 Usiseme: *Nitalipiza* uovu!
LISHA, Yoh 21:17 *Lisha* kondoo wangu wadogo
LISLOWEZEKANA, Mwa 18:14 *lisilowezekana* kwa Yehova?
LITANGAZWE, Kut 9:16 ili jina langu litangazwe
LOTI, Lu 17:32 Mkumburike mke wa *Loti*
 2Pe 2:7 alimwokoa Loti mwa dilifu,
LUGHA, Mwa 11:7 kuvuruga *lugha* yao
 Sef 3:9 nitabadili *lugha* ya mataifa iwe *lugha* safi
 Zek 8:23 watu kumi kutoka katika *lugha* zote
 Mdo 2:4 wakaanza kusema *lugha* mbalimbali
 1Ko 13:8 kama kuna *lugha*, zitakoma
 1Ko 14:22 *lugha* ni ishara kwa wasio waamini
 Ufu 7:9 mataifa yote, makabila, na *lugha*
LUKA, Kol 4:14 *Luka*, daktari mpendwa
LULU, Mt 7:6 msitwapue ngururu *lulu* zenu
 Mt 13:45 Ufalme, mfanyiabiashara akitaftua *lulu*

M

MAADILI, Efe 4:19 wamepotoka kabisa *kimaadili*
MAADUI, Zb 110:2 Nenda ukitisha kati ya *maadui* wako
MAANDIKO, Mt 22:29 hamjui *Maandiko* wala nguvu
 Lu 24:32 miyo ikiwaka alipotufungulia *Maandiko*
 Mdo 17:2 akajadiliana na alio kutimia *Maandiko*
 Mdo 17:11 wakiyachunguza *Maandiko* kwa ungalifu
 Ro 15:4 faraja kutoka kwa *Maandiko*
MABALOZI, 2Ko 5:20 *mabalози* badala ya Kristo
MABAMBA, Kut 31:18 alimpa Musa *mabamba* mawili
MABAWA, Ru 2:12 kimbilio chini ya *mabawa* yake
MABAYA, Mwa 3:5 mkijua chemu na *mabaya*
MABIKIRA, Mt 25:1 Ufalme ni kama *mabikira* kumi
 1Ko 7:25 kuhusu *mabikira*, sina amri
MABINTI, Yoe 2:28 *mabinti* wenu watotoa unabii
 Mdo 21:9 *mabinti* wanne waliotoa unabii
 2Ko 6:18 mtakuwa wana na *mabinti* kwangu
MABWANA, Mt 6:24 kuwatumikia *mabwana* wawili
 1Ko 8:5 miungu mingi na *mabwana* wengi
MACHAFUKO, 1Ko 14:33 Mungu si Mungu wa *machafuko*
MACHINJIONI, Isa 53:7 kama kondoo *machinjioni*
MACHO, 2Nya 16:9 *macho* ya Yehova, huku na huku
 Zb 115:5 zina *macho*, lakini haziwezi kuona
 Met 15:3 *Macho* ya Yehova yako kila mahali
MACHOZI, 2Fa 20:5 Nimeona *machози* yote
 Zb 6:6 ninakilowesha kitanda changu kwa *machози*
 Zb 6:6 Kochi langu linarufika *machози*
 Zb 126:5 wanaopanda mbevu kwa *machози*
 Mhu 4:1 *machози* ya wanaokandamizwa
 Mdo 20:19 nilivyotumikia *machози* na
 Mdo 20:31 kumwonya kila mmoja kwa *machози*
 Ebr 5:7 Kristo alitoa maombi kwa *machози*
MADENI, Mt 6:12 utusamehe *madeni* yetu, kama vile
MADHABAHU, Mwa 8:20 Noa alijenga *madhabahu*
 Kut 2:21 tengeneza *madhabahu* kwa mshita
 Mt 5:24 acha zawadi mbele ya *madhabahu*
 Mdo 17:23 *madhabahu* kwa Mungu Asiyejulikana
MADHARA, Zb 23:4 Siogopi *madhara* yoyote
 Met 27:12 wajinga hapata *madhara*
 Isa 11:9 Hawataasabisha *madhara* yote
MADHEHEBU, Mdo 28:22 *madhehebu*, yasemwa vibaya
 Tit 3:10 mtu anayeendelea *madhehebu*
 2Pe 2:1 wataingiza kimyakima *madhehebu*
MAELFU, Ufu 5:11 makumi ya *maelfu*
MAENDELEO, Yoh 8:37 neno langu halifanyi *maendeleo*
 Flp 3:16 kadiri ambavyo tumefanya *maendeleo*
 1Ti 4:15 *maendeleo* yaonekane wazi kwa wote
MAFUTA, 1Fa 17:16 *mafuta* hayatakwisha
 Mt 25:4 wenye busara walibeba *mafuta*
 Mk 14:4 Kwa nini *mafuta* haya ya marashi yapotezwe?
MAGARI YA VITA, Amu 4:13 *magari 900 ya vita* yenye
 2Fa 6:17 *magari ya vita* kumzunguka Elisha
MAGOGU, Eze 38:2 dhidi ya Gogu wa nchi ya *Magogu*
MAGONJWA, Isa 53:4 aliyabeba *magonjwa* yetu
 Lu 21:11 *magonjwa* katika sehemu mbalimbali
MAHAKAMA, Da 7:10 *Mahakama* ikaketi
 Mk 13:9 Watu watawapeleka *mahakamani*
 1Ko 6:6 ndugu anaenda *mahakamani* kumshtaki ndugu
MAHANGAIKO, Zb 94:19 *Mahangaiko* yaliponilemea
 Met 12:25 *Mahangaiko* hulemea moyo
 Mk 4:19 *mahangaiko* na nguvu za udanganyifu
 Lu 8:14 wanakengeushwa na *mahangaiko*
 Lu 21:34 miyo isilemewa na *mahangaiko*
MAHEKALU, Mdo 17:24 hakai katika *mahekalu*
MAHEMA, Mdo 18:3 kazi yao, kutengeneza *maHEMA*
MAHITAJI, Ro 12:13 Shirikini kulingana na *mahitaji* yao
MAJALIWA, Isa 65:11 mungu wa *Majaliwa*
MAJANI, Isa 65:25 Simba atakula *majani* kama ng'ombe
 Eze 47:12 *majani* yake yatatumia kuponya
 Mt 24:32 matawi yake yanapochipua *majani*
MAJANI MAKAVU, 1Ko 3:12 akienga kwa *majani makavu*
MAJARIBU, Mt 6:13 Na usituingeze katika *majaribu*
 Mt 26:41 kusali ili msilingie katika *majaribu*
 Lu 22:28 mmeshakamana nami katika *majaribu*
 1Ko 10:13 *majaribu* ya kawaida kwa watu
 Yak 1:2 shangwe, mnapopata *majaribu*
MAJERAHA, Met 23:29 Ni nani aliyé na *majeraha*?

Met 27:6 *Majeraha* yanayosababishwa na rafiki
Isa 53:5 kwa *majeraha* yake tuliponywa
MAJESHI, Ufu 19:14 *majeshi* ya mbinguni yakimfuata
MAJI, Hes 20:10 *maji* katika mwamba huu?
Met 20:5 Mawazo ya moyo kama *maji* wenyewe kina
Met 25:25 Kama *maji* baridi kwa nafsi iliyochocha
Isa 55:1 nyote mlio na kiu, njooi kwenye *maji*
Yer 2:13 Wameniacha, chemchemi ya *maji* yaliyo hai
Yer 50:38 *maji* yake yatakaushwa
Zek 14:8 *maji* yaliyo hai, kutoka Yerusalemu
Yoh 4:10 angekuwa *maji* yaliyo hai
1Ko 3:6 nilipanda, Apolo akatia *maji*
Ufu 7:17 kuwaongoza kwenye chemchemi za *maji*
Ufu 17:1 kahaba anayekaa juu ya *maji*
MAJJI, Lu 4:43 habari njema katika *majiji* mengine
MAJJI YA MAKIMBILIO, Hes 35:11 *majiji* ya *makimbilio*
Yos 20:2 Jichaguliene *majiji* ya *makimbilio*
MAJIRA, Da 2:21 hubadili nyakati na *majira*
Mdo 1:7 juu yenu kujua nyakati au *majira*
1Th 5:1 kuhusu nyakati na *majira*
MAJIVUNO, Yak 4:6 Mungu huwapiga wenyewe *majivuno*
MAJUMA, Da 9:24 *majuma* 70 yameamliwa
MAKAA YA MAWE, Ro 12:20 utakusanya *makaa* ya *mawe*
MAKABILA, Mwa 49:28 Hayo ndiyo *makabila* 12 ya Israeli
MAKAHABA, Lu 15:30 aliyetuma mali na *makahaba*
MAKAPI, Sef 2:2 siku hivyo haijapeperuka kama *makapi*
MAKEDONIA, Mdo 16:9 Vuka uingie *Makedonia* utusaidie
MAKERUBI, Mwa 3:24 akaweka *makerubi* na upanga
MAKUBALIANO, 1Ko 7:5 Msinyamane ila kwa *makubaliano*
MAKUHANI, Mik 3:11 *Makuhani* hufundisha kwa malipo
Mdo 6:7 umati mkubwa wa *makuhani* wakaamini
Ufu 20:6 *makuhani* wa Mungu, miaka 1,000
MAKUSANYIKO MATAKATIFU
Law 23:4 sherehe za Yehova, *makusanyiko matakatifu*
MAKUU, Ro 12:16 msikazie akili mamba *makuu*
MALAIKA, Mwa 28:12 *malaika* wakipanda na kushuka
2Fa 19:35 *malaika* aliwaua 185,000
Ayu 4:18 huona *malaika* wana kasoro
Zb 34:7 *Malaika* wa Yehova hupiga kambi
Da 3:28 alituma *malaika* wake na kuwaokoa
Ho 12:4 [Yakobo] ashindana na *malaika*
Mt 13:41 atawatuma *malaika* zake, watakusanya
Mt 22:30 ni kama *malaika* mbinguni
Mt 24:31 *malaika* watakusanya waliochaguliwa
Mdo 5:19 *malaika* afungua milango ya gereza
Mdo 12:11 alituma *malaika* na kunikomboa
1Ko 4:9 tamasha kwa *malaika*
1Ko 6:3 hamjui tutawahukumu *malaika*?
Ebr 13:2 waliwakaribisha *malaika*
1Pe 1:12 *Malaika* wanatamani kuchungulia
Yud 6 *malaika* hawakubaki mahali pao
MALAIKA MKUU, 1Th 4:16 kwa sauti ya *malaika mkuu*
Yud 9 Mikaeli, *malaika mkuu*
MALALAMIKO, Kol 3:13 sababu ya *kulalamika* juu ya
MALI, Kut 19:5 mtakuwa *mali* yangu ya pekee
Zb 62:10 *Mali* zikiongezeka, usizikazie moyoni
Met 11:4 *Mali* haitakuwa na faida siku ya ghadhabu
Met 18:11 *Mali* ya tajiri ni ukuta, mawazoni mwake
Mhu 5:10 anayependa *mali* hatatosheka na mapato
Isa 60:5 *Mali* za mataifa zitakuja kwako
Isa 61:6 Mtakula *mali* za mataifa
Lu 14:33 asipoaga *mali* zake
Lu 16:9 marafiki kupitia *mali* zisizo za uadilifu
1Ko 6:19 ninyi si *mali* yenu wenyewe
Ebr 10:34 makakubali kuporwa *mali* zenu
MALIPO, Yer 22:13 anataka kulimpa *malipo* yake
MALIZA, Mdo 20:24 *malizwa* mwendo wangu na huduma
MALKIA, 1Fa 10:1 *malkia* wa Sheba alisikia
MALTA, Mdo 28:1 kisiwa hicho kiliiwa Malta
MAMA, Kut 20:12 Msheshimu baba yako na *mama* yako
Zb 27:10 Hata baba na *mama* wakiniacha
Met 23:22 usimdharau *mama* yako kwa kuzeeka
Lu 8:21 *Mama* yangu na ndugu zangu ni hawa
Yoh 19:27 akamwambia: Ona! *Mama* yako!
Gal 4:26 Yerusalemu la juu ni *mama* yetu
MAMBO MADOGO, Zek 4:10 siku ya *mambo madogo*
MAMBO MAZITO, Mt 23:23 *mambo mazito* zaidi ya Sheria
MAMBO YA MSINGI, Gal 4:9 marudria yako ya *msingi*

MAMBO YOYOTE, Flp 4:8 *mambo yoyote* ya kweli
MAMLAKA, Met 28:16 hutumia vibaya *mamlaka*
Mt 28:18 Nimepewa *mamlaka* yote
Lu 4:6 Nitakuwa *mamlaka* hii yote na utukufu wake
Ro 13:1 ajitishie kwa *mamlaka* zilizo kubwa
1Ko 9:18 nisitumie vibaya *mamlaka*
Tit 3:1 kuzitii serikali na *mamlaka*
2Pe 2:10 wanaodharau *mamlaka*
MANA, Kut 16:31 Israeli walitua mkate huo *mana*
Yos 5:12 *Mana* ilikoma siku iliyoifuata
MANABII, 1Fa 18:4 Obadia aliwaficha *manabii* 100
Amo 3:7 huwafundisha *manabii* wake *manabii* siri
Mdo 10:43 *Manabii* wote walitua ushahidi kumhusu
MANABII WA UWONGO, Mt 7:15 *manabii* wa uwongo
Mt 24:11 *Manabii* wa uwongo watawapotosha wengi
Mk 13:22 *manabii* wa uwongo watafanya maajabu
MANASE, 2Nya 13:13 *Manase* akajua kwamba Yehova
MANENO, Met 14:23 *maneno* matupu huleta umaskini
MANENO MENGINE, 1Ko 2:1 sikuja na *maneno mengi*
MANUFAA, Kum 8:16 ili awanufaishe baadaye
2Ti 1:13 kigezo cha *maneno yenge manufaa*
Tit 2:1 yanayopatana na fundisho lenye *manufaa*
MANUNG'UNIKO, Hs 14:27 *manung'uniko* ya Waisraeli
MANYOYA, Amu 6:37 umande juu ya *manyoya* pekee
MAOMBI, Zb 20:5 Yehova na atimize *maombi* yako
MAOMBOLEZO, Mhu 7:2 kwenda kwenye *maombolezo*
MAONI, 1Fa 18:21 kuyumbayumba kati ya *maoni* mawili
Ro 14:1 mshukumu kuhusu *maoni* yanayotofautiana
MAONO, Da 10:14 *maono* kuhusu siku zijazo
MAPAJI, Eze 9:4 uyatie alama *mapaji* ya nyuso za wata
MAPAMBO, 1Pe 3:3 *Kujipamba* kweni kusiwe kwa nje
MAPATO, Mhu 5:10 hatatosheka na *mapato*
MAPENZI, Zb 40:8 nafurahia kufanya *mapenzi* yako
Zb 14:30 Nifundishe kufanya *mapenzi* yako
Mt 6:10 *Mapenzi* yako yatendeke duniani
Mt 7:21 bali anayefanya *mapenzi* ya Baba yangu
Lu 22:42 *mapenzi* yako na yatendeke
Yoh 6:38 sikuja kufanya *mapenzi* yangu
Mdo 21:14 *Mapenzi* ya Yehova na yatendeke
Ro 12:2 *mapenzi* ya Mungu yanayokubalika
Efe 1:5 kulingana na *mapenzi* yake mema
1Th 4:3 *mapenzi* ya Mungu, mijepushe na uasherati
1Yo 2:17 anayefanya *mapenzi* ya Mungu anadumu
1Yo 5:14 tukioimba kulingana na *mapenzi* yake
MAPIGO, Ufu 18:4 ikiwa hamtaki kupokea *mapigo* yake
MAPOKEO, Mt 15:3 huvunja amri kwa *mapokeo*
Mk 7:13 batilisha neno la Mungu kwa *mapokeo*
Gal 1:14 bidii ya *mapokeo* ya baba zangu
MAPYA, Isa 42:9 ninatangaza *mambo mapya*
MARAFIKI, Met 14:20 Lakini tajiri ana *marafiki* wengi
Met 16:28 mchongezi hutenganisha *marafiki*
Lu 16:9 Jifanyieni *marafiki* kupitia mali
MARIA 1, Mk 6:3 seremala mwana wa *Maria*
MARIA 2, Lu 10:39 *Maria* alikuwa akisikiliza *Bwana*
Lu 10:42 *Maria* alichagua fungu zuri
Yoh 12:3 *Maria* akachukuwa mafuta yeye marashi
MARIA 3, Mt 27:56 kulikuwa na *Maria* Magdalene
Lu 8:2 *Maria* Magdalene, aliyetolewa roho waovu
MARIA 4, Mt 27:56 na *Maria* mama ya Yakobo na Yose
MARIA 5, Mdo 12:12 *Maria* mama ya Yohana Marko
MARKO, Kol 4:10 *Marko*, binamu ya Barnaba
MARTHA, Lu 10:41 *Martha*, unahangaikia mambo mengi
MASALIO, Law 19:9 msiookote *masalio* ya mvumo yenu
Ru 2:8 Boazi, usiookote *masalio* pengine
MASHAHIDI, Kum 19:15 ushahidi wa *marshahidi* wawili
Isa 43:10 Ninyi ni *marshahidi* wangu
Mt 18:16 ushahidi wa *marshahidi* wawili au watatu
Mdo 1:8 mtakuwa *marshahidi* wangu katika
Ufu 11:3 *marshahidi* wawili wote unabii siku 1,260
MASHAMBA, Isa 65:21 *marshamba* ya mizabibu
Yoh 4:35 mtazame *marshamba*, ni neupe
MASHARIKI, Isa 41:2 amemwinua mtu kutoka *marshariki*
MASHINDANO, Gal 5:26 tusiochonge *marshindano*
MASHIRIKIA, Angalia SHIRIKIANA.
MASHTAKA, 1Ko 6:7 *mashtaka* ya kisheria
MASHUHURI, 1Ko 1:26 si wengi wa familia *mashuhuri*
MASHIHI, Da 9:25 mpaka atakapotekea *Mashihi*, Kiongozi
Da 9:26 baada ya majuma 62, *Mashihi* atauawa

Yoh 1:41 Tumempata *Masihi*
 Yoh 4:25 Ninajua kwamba *Masihi* anakuja
MASIKIO, 2Ti 4:3 *masikio* yu yafurahishwe
MASKINI, 1Sa 2:8 Humwina *maskini* kutoka majivu
 Zb 9:18 *maskini* hawatasahauliwa daima
 Zb 69:33 Yehova anawasiliza *maskini*
 Met 30:9 wala niwe *maskini*, niibe na kuliaibisha
 Lu 4:18 niwatangazie *maskini* habari njema
 Yoh 12:8 *maskini* mnao sikuzote
 Ro 7:24 *Maskini* mim!
 2Ko 6:10 *maskini* lakini wanaowatajirisha wengi
 2Ko 8:9 Kristo alikuwa *maskini* kwa ajili yenu
 Gal 2:10 tuwakumbuke *maskini*
MASURIA, 1Fa 11:3 wake 700 na *masuria* 300
MASWALI, 1Ti 1:4 hutokeza *maswali*
MATAIFA, Mwa 22:18 *Mataifa* yote yatajipatia baraka
 Mt 25:32 *Mataifa* yote yatakusanyika mbele yake
 Lu 21:24 nyakati zilizowekwa za *mataifa* zitimie
MATAJIRI, Law 19:15 usiwapendelee *matajiri*
 Lu 14:12 Unapoandaa mlo usiwaite *matajiri*
 1Ti 6:9 wamezimia kuwa *matajiri* huanguka
 1Ti 6:17 walio *matajiri* wasijivune
MATARAJIO, Met 13:12 *Matarajio* yaliyoahirishwa
 Hab 2:3 Hata yakikawia, endelea *kyutarajial*
 Lu 1:15 watu walikuwa *wakitarajia*
 Lu 21:26 watazimia kwa woga *wakitarajia* mambo
MATATIZO, Zb 34:19 Mwadilifu ana *matatizo* wengi
MATENDO YALIYOKUFA, Ebr 9:14 *matendo yaliyokufa*
MATESO, Zb 119:50 faraja yangu katika *mateso*
 Mt 13:21 *mateso* yakitokea mara moja anakwazika
 Mk 4:17 wanapopata *mateso*, wanakwazika
 Mk 10:30 watoto, mashamba, pamoja na *mateso*
 Ro 8:18 *mateso* ya wakati huu si kitu
 2Th 1:4 uvumilivu na imani yenu katika *mateso*
 Ebr 2:10 Wakili Mkuu, mkamilifu kupitia *mateso*
 1Pe 5:9 *mateso* yaleyale yanaupata ushirika
MATITI, Met 5:19 *Matiti* yake na yakuridhishe
MATOFAA, Met 25:11 *matofaa* ya dhahabu
MATOKEO, Isa 46:10 Tangu mwanzo ninatabiri *matokeo*
 Isa 55:11 neno langu halitarudi bila *matokeo*
MATOLEO, 1Nya 29:9 walishangilia, walitoa *matoleo*
MATOWASHI, Isa 56:4 *matowashi*, wanaoshika sabato
 Mt 19:12 *matowashi* kwa ajili ya Ufalme wa mbinguni
MATUNDA, Mwa 3:3 *matunda*, wala msiyaguse
 Mt 7:20 mtawatambua kwa *matunda* yao
 Mt 21:43 kupewa taifa linaloza *matunda*
 Lu 8:15 kuzaa *matunda* kwa uvumilivu
 Yoh 15:2 hulisafisha ili lizae *matunda* zaidi
 Yoh 15:8 hutukuzwa mnapozaa *matunda* mengi
 Ro 8:23 sisi tulio na *matunda* ya kwanza
MATUSI, Efe 4:31 ghadhabu, kufoka, na *matusi*
MAUMBILE, Yud 7 tamaa zilizo kinyume cha *maumbile*
MAUMIVU, Ayu 6:2 *maumivu* yangu yangepimwa
 Met 17:25 Mwana mpumbavu huleta *maumivu*
 Ro 8:22 umbaji unaugua katika *maumivu*
 Ro 9:2 huzuni na *maumivu* yasiyoisha moyoni
MAUMIVU MAKALI, Lu 21:25 *mataifa*, *maumivu* makali
MAVAZI, Mwa 3:21 Mungu akatengeneza *mavazi* marefu
 Efe 6:11 *mavazi* kamili ya silaha
MAVAZI KAMILI, Efe 6:13 *mavazi kamili* ya silaha
MAVUMBI, Mwa 2:7 akamuumba kwa *mavumbi*
 Mwa 3:19 wewe ni *mavumbi* nawe utarudi *mavumbini*
 Zb 103:14 Akikumbuka kwamba sisi ni *mavumbi*
 Isa 40:15 *Mataifa* ni kama *mavumbi* membamba
MAVUNO, Mt 9:37 *mauvuno* ni mengi
MAWAZO, Zb 26:2 Safisha *mawazo* yangu ya ndani
 Zb 139:17 *mawazo* yako ni yenye thamani
 Zb 146:4 Siku hiyo *mawazo* yake hupotea
 Met 20:5 *Mawazo* moyoni kama maji yenye kina
 Isa 55:8 *mawazo* yangu si *mawazo* yenu
Mawe, Lu 19:40 wakinyamaza, *mawe* yatapaza sauti
MAWINGU, Mhu 11:4 anayetazama *mawingu* hatavuna
 Mt 24:30 Mwana wa binadamu akija juu ya *mawingu*
MAYATIMA, Yak 1:27 kuwazuna *mayatima* na wajane
MAYUNGIYUNGI, Lu 12:27 Angaliani *mayinguniyungi*
MAZIWA, Kut 3:8 nchi inayotiririka *maziwa* na asali
 Isa 60:16 utakunywa *maziwa* ya mataifa

Ebr 5:12 mnahitaji *maziwa* tena
 1Pe 2:2 hamu kwa ajili ya *maziwa* yasiyochanganywa
MAZOEFA, 1Yo 3:6 hana *mazoea* ya dhambi
MAZOEZI, 1Pe 5:10 Mungu atamaliza *mazoezi* yenu
MBEGU, Lu 8:11 *Mbegu* ni neno la Mungu
MBINGU, Zb 8:3 Ninapoziona *mbingu* zako
 Zb 19:1 *Mbingu* zinatangaza utukufu wa Mungu
 Yoh 3:13 hakuna mtu aliyependa *mbinguni*
 2Ko 12:2 alinyakuliwa mpaka *mbingu* ya tatu
 2Pe 3:13 tunangojia *mbingu* mpya na dunia mpya
MBINU, 2Ko 2:11 hatukosi kujizua *mbinu* zake
MBIO, Mhu 9:11 si wenye *mbio* wanaoshinda *mbio*
 2Ti 4:7 nimekimbia *mbio* mpaka mwisho
MBONI, Zb 17:8 Nilinde kama *mboni* ya jicho lako
 Zek 2:8 anaigusa *mboni* ya jicho langu
MBUZI, Mt 25:32 anavyotenganisha kondoo na *mbuzi*
MBWA, Mt 26:17 mtu anayemkamata *mbwa* masikio
 Mhu 9:4 *mbwa* aliye hai ni afadhali kuliko
 2Pe 2:22 *Mbwa* ameyarudia matipishi yake
MBWAMWITU, Isa 11:6 *Mbwamwitu* atakaa na
 Mt 7:15 *mbwamwitu* katika mavazi ya kondoo
 Lu 10:3 wanakondoo katikati ya *mbwamwitu*
 Mdo 20:29 *mbwamwitu* wenye kukandamiza
MBWEHA, Mt 8:20 *Mbweha* wana mapango, lakini
MCHANGA, Mwa 22:17 uzao wako kama *mchanga*
 Ufu 20:8 Idadi yuo, *mchanga* wa bahari
MCHANGAMFU, 2Ko 9:7 mtoaji *mchangamfu*
MCHezo, Mt 10:23 kama *mchezo* kwa mpumbavu
MCHONGEZI, Met 16:28 *mchongezi* hutenganiha
MCHOYO, Mt 23:6 Usile chakula cha mtu *mchoyo*
MCHUNGAJI, Zb 23:1 Yehova ni *Mchungaji* wangu
 Isa 40:11 Atalitunza kundi kama *mchungaji*
 Eze 37:24 Daudi *mchungaji* mmoja
 Zek 13:7 Mpijia *mchungaji*, kondoo watawanyike
 Mt 9:36 kama kondoo wasio na *mchungaji*
 Yoh 10:11 *mchungaji* mwema hutooa uhai wake
 Yoh 10:14 Mimi ndiye *mchungaji* mwema
 Yoh 10:16 kundi moja, *mchungaji* mmoja
MDOGO, Isa 60:22 *Mdogo* atakuwa elfu
 Lu 9:48 anayejijendesha kama *mdogo* zaidi
MELI, 2Ko 11:25 mara tatu nilivunjikiwa na *meli*
MELKIZEDEKI, Mwa 14:18 *Melkizedeki* mfalme wa
 Zb 110:4 kuhani milele mfuno wa *Melkizedeki*
MEMA, Mwa 3:5 kama Mungu, mkijua *mema* na mabaya
 Gal 6:10 tuwatendee watu wote *mema*
MENGI, 1Ko 15:58 mkwiwa na mengi katika kazi ya Bwana
MEZA, Da 11:27 kwenye *meza* moja wakidanganyana
 1Ko 10:21 kushiriki *meza* ya Yehova na
MFALME, Amu 21:25 hakukuwa na *mfalme* Israeli
 1Sa 23:17 utakuwa *mfalme*, nami nitakuwa wa pili
 Zb 2:6 nimeuwaka *mfalme* wangu
 Met 21:1 Moyo wa *mfalme* ni kama vijito
 Isa 32:1 *Mfalme* atatawala kwa uadilifu
 Zek 14:9 Yehova atakuwa *Mfalme* juu ya dunia yote
 Mt 21:5 *Mfalme* wako anakuja, juu ya punda
 Mt 27:29 Salamu, ewe *Mfalme* wa Wayahudi!
 Yoh 19:15 hatuna *mfalme* ila Kaisari
 1Ko 15:25 lazima atawale akiwa *mfalme* mpaka
MFALME WA KASKAZINI, Da 11:7 *mfalme* wa kaskazini
 Da 11:40 *mfalme* wa kaskazini atamshambulia
MFALME WA KUSINI, Da 11:11 *mfalme* wa kusini
 Da 11:40 *mfalme* wa kusini atasukumana naye
MFANO, Mwa 1:26 tumuume mtu kwa *mfano* wetu
 1Ti 4:12 uwe *mfano* mzuri kwa waaminifu
 Yak 5:10 fuatani *mfano* wa manabii
MFANYABIASHARA, Mt 13:45 *mfanyabiashara*, lulu
MFANYAKAZI, Met 8:30 kando yake, *mfanyakazi* stadi
 Lu 10:7 *mfanyakazi* anastahili mshahara wake
MFINYANZI, Isa 64:8 nawe ni *Mfinyanzi* wetu
 Ro 9:21 je, *mfinyanzi* hama mamlaka
MFUASI, Mt 19:21 uje uwe *mfuasi* wangu
MFUPA, Mwa 2:23 huyu ni *mfupa* wa mifupa yangu
 Met 25:15 ulimi laini unaweza kuujiwa *mfupa*
 Yoh 19:36 Hakuna *mfupa* utakaovunjwa
MGAWANYIKO, Mt 10:35 nilikuja kuleta *mgawanyiko*
MGENI, Hes 9:14 sheria moja kwa *mgeni* na mwenyeji
 Zb 15:1 nani atakuwa *mgeni* katika hema lako?

MGONJWA, Isa 33:24 atakayesema: Mimi ni *mgonjwa*

Yak 5:14 kuna yeyote aliye *mgonjwa*

MGUMU, Ebr 3:13 asifanya *mgumu* na dhambi

MHUBIRI, 2Pe 2:5 Noa, *mhubiri* wa uadilifu

MHUDUMU, 1Sa 2:11 akawa *mhudumu* wa Yehova

Mk 10:43 mkubwa taji wenu awe *mhudumu*

MIAKA 50, Law 25:10 Mwadhimisho wa *Miaka 50*

MIANGA, Flp 2:15 mnaangaza kama *mianga*

MICHANGO, 2Nya 31:10 walipoanza kuleta *michango*

MIDOMO, Met 10:19 anayedhibiti *midomo* ana busara

Isa 29:13 huniheshimu kwa *midomo* yao

Ho 14:2 tutatota sifa ya *midomo* yetu

Ebr 13:15 dhahibu ya sifa, tunda la *midomo*

MIFANO, Mt 13:34 Yesu alizunguma kwa *mifano*

Mk 4:2 akaanza kuwafundisha kwa *mifano*

MIFUGO, Isa 30:23 *mifugo* yenu italisha malisho

MIFUPA, 2Fa 13:21 aliyegusa *mifupa* ya Elisha

Zb 34:20 Atailinda *mifupa* yake

Yer 20:9 kama moto uliofunguwa *mifupani* mwangu

MIGAWANYIKO, Ro 16:17 wanaasababisha *mgawanyiko*

1Ko 1:10 kusiwe na *mgawanyiko* kati yenu

MIGUMU, Mk 3:5 akuhuzunisha na *mioyo migumu*

MIGUU, Isa 52:7 inavyopendelea *miguu* ya anayeleta

Yoh 13:5 akaanza kuioha *miguu* ya wanafunzi

Ro 16:20 atamponda *Shetani* chini ya *miguu* yenu

MIBA, Mk 15:17 wakasokota taji la *miba* wakamvisha

MILLI, Ro 6:13 toeni *milli* yenu kwa Mungu

Ro 12:1 mtee *milli* yenu iwe dhahibu *iliko* haki

MIKAELI, Da 10:13 *Mikaeli*, mmoja wa wakuu wenye vyeo

Da 12:1 Wakati huo *Mikaeli* atasimama

Ufu 12:7 *Mikaeli* na malaika zake wakapigana

MIKONO, Isa 35:3 Itieni nguvu *mikono* iliyo dhifu

MIKONO MITUPU, Kum 16:16 *mikono mitupu*

MILANGO, Yoh 20:19 akaja *milango* ikiwa imefungwa

MILELE, Mwa 3:22 ili asile matunda na kuishi *milele*

Zb 37:29 Waadilifu wataishi duniani *milele*

Mhu 3:14 kazi za Mungu zitadamu *milele*

1Pe 1:25 neno la Yehova linadamu *milele*

MILIMA, Mwa 7:20 Maji yalipanda juu ya *milima*

MIMBA, Kut 21:22 kumuunika mwenye *mimba*

Kut 23:26 hakuna *mimba* itakayoharibika

1Th 5:3 maumivu wa mwanamke mwenye *mimba*

MINA, Lu 19:16 *mina* yako imeleta faida ya *mina* kumi

MIOYO, Met 17:3 Yehova ndiye mchunguzaji wa *mioyo*

Lu 12:34 ilipo hazina yenu, ndipo *mioyo* itakapokuwa

Lu 21:34 *mioyo* yenu isilemwe kamwe

Lu 24:32 *mioyo* yetu iliwaka akizunguma nasi

1Yo 3:20 Mungu ni mkuu kuliko *mioyo*

MIPAKA, 1Th 4:6 yeyote asivuke *mipaka* inayofaa

MIPANGO, Met 15:22 *Mipango* huvunjika

Met 19:21 Moyo wa mwanadamu una *mipango* mingi

MIRIAMU, Hes 12:1 *Miriamu* na Haruni dhidi ya Musa

MISHALE, Zb 127:4 Kama *mishale* mkononi mwa

MISRI, Mt 2:15 Nikamwita mwanangu atoke *Misri*

MITI, Isa 61:3 wataitwa *miti* mkubwa ya uadilifu

Eze 47:12 Aina zote za *miti* kwenye kingo zote

Ufu 22:14 mamlaka kwenda kwenye *miti* ya uzima

MITUME, Mt 10:2 majina ya wale *mitume* 12

Mdo 15:6 *mitume* na wazee wakacusanyika kulichunguza

1Ko 15:9 mimi ni mdogo zaidi kati ya *mitume*

2Ko 11:5 *mitume* wenu walio bora sana

MIZANI, Law 19:36 Mnapaswa kutumia *mizani* sahihi

Met 11:1 *Mizani* ya uwongo huchukiza Yehova

MIZIGO, Gal 6:2 kubebeana *mizigo*

MIZIZI, Lu 8:13 hupokea kwa shangwe, hawana *mizizi*

Kol 2:7 mkiwa mmetia *mizizi* na kujengwa

MJANE, Zb 146:9 Humtegemeza yatima na *mjane*

Mk 12:43 *mjane* maskini ametoa zaidi ya wote

Lu 18:3 *mjane* aliyekuwa akienda kumwomba

MJINGA, Met 14:15 *Mjinga* huamini kila neno

MJUMBE, Mal 3:1 Ninamta *mjumbe* kwaingii

MKAAJI MGENI, Kut 22:21 Msimtee *mkaaji mgeni*

Kum 10:19 lazima mumpende *mkaaji mgeni*

MKAMILIFU, Mt 5:48 Baba yenu alivyo *mkamilifu*

Ebr 2:10 Wakili Mkuu *mkamilifu* kupitia mateso

MKARIMU, Met 11:25 *mkarimu* tatupa ufanisi

MKATE, Ne 9:15 uliwapu *mkate* kutwapa mbinguni

Zb 37:25 wala watoto wake wakitafuta *mkate*

Isa 55:2 kila nini mlipie kiti ambacho si *mkate*

Mt 4:4 Mwanadamu hataishi kwa *mkate* tu

Mt 6:11 Utupatie leo *mkate* wetu

Mt 26:26 Yesu akachuka *mkate*, akaumega

Yoh 6:35 Mimi ndio *mkate* wa uzima

1Ko 10:17 *mkate* mmoja, tunakula *mkate* huo

MKATILI, Met 11:17 mtu *mkatili* hujiletea shida

Met 12:10 rehema ya waovu ni *ukatili*

MKAZO, 1Sa 1:15 mwanamke mwenye *mkazo* mkubwa

2Ko 1:8 Tulikuwa na *mkazo* mkubwa sana

MKE, Mwa 2:24 atashikamana na *mke* wake

Mwa 27:46 Yakobo akioa *mke* kwa mabinti

Met 5:18 shangilia na *mke* wa ujana wako

Met 12:4 *Mke* mwema ni taji kwa mume wake

Met 18:22 Anayepata *mke* mwema hupata kibali

Met 21:19 Kuliko kuishi na *mke* mgomvi

Met 31:10 nani anaweza kumpata *mke* mwema

Mhu 9:9 Furahia maisha na *mke* mpendwa

Mal 2:15 usimteeke hila *mke* wa ujana wako

1Ko 7:2 kila mwanamume na awe na *mke* wake

1Ko 9:5 kuambatana na *mke* mwamini

MKONO, Zb 145:16 Unaufumbua *mkono* wako

Isa 41:10 Nitakushika kwa *mkono* wangu wa kuume

Zek 14:13 ataukamata *mkono* wa mwenzake, na *mkono*

Mt 6:3 *mkono* wa kushoto usiye *mkono* wa kulia

Mt 6:27 kurefusha uhai kwa *mkono* mmoja?

Yoh 12:38 *mkono* wa Yehova, umefunuliwa kwa nani?

MKOPAJI, Met 22:7 *mkopaji* ni mtumwa wa mkopeshaji

MKOPO, Met 11:15 anamwheka dhama na *mkopo*

MKUKI, 1Sa 18:11 akamrusiwa Daudi *mkuki*

MKUSANYA KODI, Mt 18:17 awe kama *mkusanya kodi*

Lu 18:11 nakushukuru mimi si kama *mkusanya kodi*

MKUU, Isa 9:6 Jina lake litakuwa *Mkuu* wa Amani

Da 10:13 *mkuu* wa Uajemi alinipiga siku 21

Yoh 14:28 Baba ni *mkuu* kuliko mimi

1Yo 3:20 Mungu ni *mkuu* kuliko mioyo yetu

MLANGO, 1Ko 16:9 *mlango* mkubwa unaongoza

Ufu 3:20 Nimesimama *mlangoni* na ninapiga hodi

MLEVI, Mt 23:21 *mlevi* na mlawi watakuwa maskini

1Ko 5:11 mwache kushirikiana na *mlevi*

MLIMA, Zb 24:3 kuupanda *mlima* wa Yehova

Isa 2:3 twendeni kwenye *mlima* wa Yehova

Isa 11:9 Wala uharibifu katika *mlima* wangu

Da 2:35 likawa *mlima* mkubwa, likaijaza dunia

MLIMA WA MIZEITUNI, Lu 22:39 *Mlima wa Mizeituni*

Mdo 1:12 *Mlima wa Mizeituni*, Yerusalemu

MLIPENI, Mt 22:21 *mlipeni* Kaisari vitu vya Kaisari

MLO WA JIONI, 1Ko 11:20 *Mlo wa Jioni* na Bwana

MLOZI, Mdo 13:6 Bar-Yesu, aliyekuwa *mlozi*

MMOJA, 1Ko 8:6 Mungu *mmoja*, Bwana *mmoja*, Kristo

MMUNG'UNYE, Yon 4:10 Uliuhurumia *mmung'unye*

MNARA, Mwa 11:4 tujijenge jiji na *mnara*

Met 18:10 Jina la Yehova, *mnara* nwenye nguvu

Lu 13:4 18 walioangukiwa na *mnara*, Siloamu

MNARA WA MLINZI, Isa 21:8 juu ya *mnara wa mlinzi*

MNYAMA, Mwa 7:2 chukua *nyama* safi saba saba

Law 18:23 kufanya ngono na *mnyama*

MNYENYEKEVU, Zek 9:9 *mnyenyekevu* juu ya punda

MOTO, Yer 20:9 kama *moto* mifupani mwangu

Mt 25:41 *moto* wa milele aliotayarisha *mbili*

1Ko 13:13 kazi itafunuliwa kupitia *moto*

1Th 5:19 Msuzime *moto* wa roho

2Ti 1:6 chochea kama *moto* zawadi iliyo ndani yako

2Pe 3:7 mbingu, dunia zimeweka kwa ajili ya *moto*

MOYO, Mwa 6:15 kila mwelekeo wa *moyo* wake

Kum 6:6 Maneno haya yawe *moyoni* mwako

1Fa 8:38 anajua matata yalio katika *moyo* wake

1Nya 28:9 kumtumikia Mungu kwa *moyo* kamili

2Nya 16:9 *moyo* wao ni kamili kumwelekea

Ezr 7:10 Ezra alitayarisha *moyo* wake

Zb 51:10 Umba *moyo* safi ndani yangu

Zb 51:17 *Moyo* uliofunjika na kupondeka hutaukataa

Met 4:23 Ulinde *moyo* wako, humo ndimo zinamotoka

Met 17:22 *Moyo* wenyewe shangwe ni dawa nzuri

Met 28:26 anayetumaina *moyo* wake ni mpumbavu

Yer 17:9 *Moyo* ni wenyewe hila kuliko kiti kingine

Yer 17:10 Mimi, Yehova, ninauchunguza moyo
 Yer 31:33 nitaandika sheria katika moyo wao
 Mt 15:19 moyoni hutoka uzini, uasherati, wizi
 Mt 22:37 Yehova Mungu wako kwa moyo wote
 Mdo 16:14 akaufungua moyo wake asikilize Paulo
 Ro 6:17 mmekuwa wataifu kutoka moyoni
 Ebr 3:12 moyo mwovu unaokosa imani usisitawi
MPAJI-SHERIA, Yak 4:12 Kuna mmoja tu *Mpaji-sheria*
MPAKA, Zb 119:96 amri yako haina *mpaka*
MPANGILIO, 1Ko 15:23 *mpangilio* wake unaofaa: Kristo
MPANGO, 1Ko 14:40 kwa adabu na *mpango*
MPATANISHI, 1Ti 2:5 *mpatanishi* kati ya Mungu na
MPENDWA, Mt 3:17 Mwanangu *mpendwa*
MPIGA RAMLI, Kum 18:11 *mpiga ramli*
MPOLE, 2Ti 2:24 anahitaji kuwa *mpole* kwa wote
MPUMBAVU, Zb 14:1 *Mpumbavu*: usikua Yehova
 Lu 12:20 Wewe *mpumbavu*, ukiu huu
MPYA, Yoh 13:34 Ninawapa ninyi amri *mpya*
 Ufu 21:1 mbingu *mpya* na dunia *mpya*
MSAADU, Zb 46:1 Msaada unapatikana kwa urahisi
MSAFISHAJI, Mal 3:3 kama *msafishaji* na mtakasaji
MSAIDIZI, Yoh 14:16 atawapa *msaidizi* wmwine
 Yoh 14:26 *msaidizi*, roho takatifu, itawafundisha
MSAMARIA, Lu 10:33 *Msamaria* akasikitika
 Yoh 4:7 Mwanamke *Msamaria* akaja kuteka maji
MSHAHARA, Mwa 31:7 kubadili *mshahara* mara kumi
 Ro 6:23 *mshahara* wa dhambi ni kifo
MSHAURI, Isa 9:6 Jina lake litakuwa *Mshauri* wa Ajabu
MSHIKAMANIFU, 2Sa 22:26 Kwa *mshikamanifu*
 Zb 16:10 Hutamruhusu *mshikamanifu* aone shimo
MSHIPI, Isa 11:5 Uadilifu utakuwa *mshipi*
MSHTAKI, Ufu 12:10 *mshakti* wa ndugu zetu ametupwa
MSIBA, Hes 23:23 ishara za *msiba* dhidi ya Yakobo
MSICHANA, 2Fa 5:2 walimchukua mataka *msichana*
 Mk 5:42 *msichana* akasimama akanza kutembea
MSIFUNI YAH, Zb 146:1 *Musifuni Yah!* Nafsi yangu yote
 Zb 150:6 Kila kitu kinachopumua—*Musifuni Yah*
 Ufu 19:1 umati mbinguni ukamesa: *Musifuni Yah!*
MSIMAMIZI, Lu 12:42 ni nani *msimamizi* mwaminifu
MSINGI, Mt 25:34 uliotayarishwa tangu kuwekwa *msingi*
 Lu 6:48 kuweka *msingi* kwenye mwamba
 Ro 15:20 nisijenge juu ya *msingi* wa mtu mwingine
 1Ko 3:11 hakuna *msingi* wowote zaidi ya
 1Pe 5:10 Mungu atawapa *msingi* imara
MSINYIMANE, 1Ko 7:5 Msiwe *msinyimane*
MTAKATIFU, Ufu 4:8 *Mtakatifu*, *mtakatifu*
MTAWALA, Da 4:17 Aliye Juu Zaidi ni *Mtawala*
 Yoh 12:31 *mtawala* wa ulimwengu huu atatupwa nje
 Yoh 14:30 *mtawala* wa ulimwengu anakuja
MTAZAMO, Efe 6:7 *mtazamo* mzuri, kama kwa Yehova
 Flp 2:5 *mtazamo* wa akili alikuwa nao Kristo
MTEGO, Zb 91:3 *mtego* wa mwindaji wa ndege
 Met 29:25 Kuwaogopa wanadamu ni *mtego*
 Lu 21:34, 35 siku ile iwakute ghafla kama *mtego*
MTENDA DHAMBI, Lu 15:7 *mtenda dhambi* anapotubu
 Lu 18:13 Mungu, nihurumie mimi *mtenda dhambi*
MTHAWABISHAJI, Ebr 11:6 huwa *mthawabishaji* wa
MTI, Mwa 2:9 *mti* wa ujuzi wa mema na mabaya
 Mwa 2:9 *mti* wa uzima katikati ya bustani
 Zb 1:3 kama *mti* uliopandwa kando ya maji
 Da 4:14 Ukateni na kuangusha *mti* huu
 Mk 15:25 wakamtundika kwenye *mti*
 Lu 23:21 Atundikwe *mtini!*
 Gal 3:13 Amelaaniwa aliyetundikwa kwenye *mti*
 Ufu 2:7 ruhusa kula matunda ya *mti* wa uzima
MTIFU, 1Fa 3:9 mpe mtumishi wako moyo *mtifu*
 Flp 2:8 alijinyenyekeza na kuwa *mtifu* mpaka kifo
MTINI, 1Fa 4:25 kua usalama, chini ya *mtini* wake
 Mik 4:4 Wataketi kila mtu chini ya *mtini* wake
 Mt 21:19 Mara moja ule *mtini* ukanyauka
 Mk 13:28 jifunzeni kutokana na *mtini*
MTI WA MATEO, Mt 10:38 *mti wa mateo*
 Lu 9:23 aubebe *mti* wa *mateo* na kunifuata
MTO, Ufu 12:16 dunia ikauzema *mto*
 Ufu 22:1 *mto* wa maji ya uzima
MTOTO, Kum 7:14 hakuna atakayekosa *mtoto*
 Amu 13:8 atufundishe jinsi ya kumlea *mtoto*

Lu 9:47 akachukua *mtoto* na kumsimamisha
 1Ko 13:11 nikifikiri kama *mtoto*, nikiwaza kama *mtoto*
MTUKUFU, Mdo 24:3 ewe *Mtukufu* Feliksi
MTUMISHI, Isa 42:1 *Mtumishi* wangu, ninayemtegemeza!
MTUMWA, Met 22:7 mkopaji ni *mtumwa* wa mkopeshaji
 Mt 24:45 *mtumwa* mwaminifu mwenye busara
 Mt 25:21 Vema, *mtumwa* mwema na mwaminifu
 Yoh 8:34 anayetenda dhambi ni *mtumwa*
 Flp 2:7 akachukua umbo la *mtumwa*
MUDA, Zb 30:5 hasira yake ni ya *muda* mfupi
 Isa 26:20 Jificheni kwa *muda* mfupi
 Ebr 11:13 walikuwa wakaajwa ya *muda*
 Ebr 11:25 kufurahia dhambi kwa *muda*
MUHIMU, Flp 1:10 mhakikishe mambo *muhimu* zaidi
MUHURI, Wim 8:6 Niweke kama *muhuri* moyoni
 Da 12:9 maneno yatiwe *muhuri* mpaka mwisho
 2Ko 1:22 ametia *muhuri* juu yetu, rehani
 Efe 1:13 Baada ya kuamini, mitiwa *muhuri*
 Ufu 7:3 hadi tuwatie *muhuri* watumwa
MUME, 1Ko 7:2 kila mwanamke awe na *mume* wake
 1Ko 7:14 *mume* asiyeamini hutakawa na mke wake
MUNGU, Kum 10:17 Yehova *Mungu* ni wa miungu
 Mt 27:46 *Mungu* wangu, kwa nini umeniacha?
 Yoh 1:18 Hakuna mwanadamu amemwona *Mungu*
 Yoh 17:3 wakujue wewe, *Mungu* wa pekee wa kweli
 Yoh 20:17 Ninapanda kwa *Mungu* wangu na *Mungu*
 1Ko 8:4 hakuna *Mungu* isipokuwa mmoja
 2Ko 4:4 *Mungu* wa mfumo huu wa mambo
 Efe 4:6 *Mungu* mmoja ambaye ni Baba wa wote
 1Yo 4:8 *Mungu* ni upendo
MUSA, Hes 12:3 *Musa* alikuwa mpole zaidi kuliko wote
 Zb 106:32 mambo yakamwendea *Musa* vibaya
 Mdo 7:22 *Musa*, mwenye nguvu katika maneno
 2Ko 3:7 hawakuweza kutazama wao wa *Musa*
MUUAJI, Yoh 8:44 Alikuwa *muuaji* alipoanza
MUUMBA, Mhu 12:1 mkumbuke *Muumba* wako
MUZIKI, Angalia NYIMBO.
MVI, Met 16:31 Mimi ni taji la umaridadi
MVIVU, Met 6:6 Mwendie chungu, ewe *mvivu*
 Met 10:26 moshi machoni, ndivyo mtu *mvivu*
 Met 19:24 *Mvivu* hutumbukiza mkono katika bakuli
 Met 20:4 *Mvivu* halimi katika majira ya baridi
 Mt 25:26 *Mtumwa* mwovu na *mvivu*
MVUA, Mwa 7:12 *mvua* ikamwagika kwa siku 40
 Kum 11:14 nitawapa *mvua* ya vuli na ya
 Kum 32:2 Mfundisho yatanyesha kama *mvua*
 Isa 55:10 kama *mvua* na theluji inavyomwagika
 Mt 5:45 *mvua* juu ya waadilifu na wasio waadilifu
MVULANA, Met 22:6 Mzoeze *mvulana* njia anayopaswa
 Isa 11:6 *mvulana* mdogo atawaongoza
 Yer 1:7 Usiseme, Mimi ni *mvulana* tu
MWADILIFU, Mwa 15:6 akamhesabu kuwa *mwadilifu*
 Zb 34:19 *Mwadilifu* ana matatizo mengi
 Zb 37:25 sijamwona *mwadilifu* akiwa amechwa
 Zb 72:7 Katika siku zake *mwadilifu* atasitawi
 Zb 141:5 *Mwadilifu* akinipiga, hilo litakuwa
 Met 24:16 *mwadilifu* anaweza kuanguka mara saba
MWAFIKIRIE, 1Th 5:13 *mwafikirie* kwa njia inayozidi
MWAGA, Zb 62:8 *Mwagani* miroye yenu mbele zake
MWAKA, Hes 14:34 siku 40, siku moja kwa *mwaka*
MWAKILISHI, Yoh 7:29 mimi ni *mwakilishi* kutoka kwake
MWAMBA, Kum 32:4 *Mwamba*, kazi zake ni kamilifu
 Mt 7:24 aliyengeja nyumba kwenye *mwamba*
MWAMINIFU, Lu 16:10 *mwaminifu* katika liliyo dogo
 1Ko 4:2 kinachotarajiwa ni kupatwa wakiwa *mwaminifu*
 1Ko 10:13 Mungu ni *mwaminifu*
 Ufu 2:10 Uwe *mwaminifu* hata kufikia kifo
MWAMUZI, Isa 33:22 Yehova ni *Mwamuzi* wetu, Mfalme
 Lu 18:2 *mwamuzi* ambaye hakumwogopa Mungu
MWANA, Zb 2:12 Mheshimuni *mwana* wa Mungu
 Met 13:24 anayeziua fimbo anamchukua *mwana*we
 Met 15:20 *Mwana* mwenye hekima humfurahisha
 Mt 3:17 Huyu ni *Mwanangu*, *mpendwa*
 Lu 15:13 *mwana* mdogo aharibu mali yake
MWANADAMU, Zb 8:4 *Mwanadamu* anayezeza kufika
MWANAJESHI, 2Ti 2:4 *mwanajeshi* haijishushiki katika
MWANAKONDOO, 2Sa 12:3 *mwanakondoo* mmoja tu
 Yoh 1:29 Ona, *Mwanakondoo* wa Mungu

MWANAMKE, Mwa 3:15 uadui kati yako na *mwanamke*
 Mhu 7:26 *Mwanamke* anayetia uchungu kuliko kifo
 Ufu 12:1 *Mwanamke* aliyepambwa jua

MWANAMUME, Law 20:13 *Mwanamume* akilala na
MWANASIMBA, Zb 91:13 Utamkanyaga *mwanasimba* na
MWANA WA BINADAMU, Da 7:13 *mwana wa binadamu*
 Mt 10:23 kabla *Mwana wa binadamu* kufika
 Lu 21:27 *Mwana wa binadamu* katika mawingu

MWANGALIZI, 1Ti 3:1 anajitahidi kuwa *mwangalizi*
 1Pe 2:25 mchungaji na *mwangalizi* wa nafsi zenu

MWANZO, Isa 46:10 Tangu mwanzo ninatamani matokeo
 Zek 4:10 dharau siku *inayoanza* kwa mambo madogo
 Mt 24:8 hayo yote ni *mwanzo* wa maumivu

MWASI IMANI, Met 11:9 *mwasi imani* humwagamiza
MWEKUNDU, Mwa 25:30 nipe mchuzi *mwekundu*
MWELEKEO, Mwa 8:21 *mwelekeo* ni mba ya tangu ujana
 1Nya 28:9 Mungu hutambua kila *mwelekeo* wa fikira
 Flp 2:20 sina mwingine aliyepambwa na *mwelekeo* kama

MWELEKEZO, Met 11:14 *Mwelekezo* stadi

MWEMA, Ro 5:7 anaweza kufa kwa ajili ya mtu *mwema*

MWENDO, Mwa 33:14 *mwendo* wa mifugo na watoto
 Yoe 2:7 Kila mmoja anafuata *mwendo* wake
 Mdo 20:24 nimalize *mwendo* wangu na huduma

MWENENDO, Gal 6:16 kanuni hii ya *mwenendo*
 1Pe 2:12 Dumishi *mwendo* mzuri kati ya mataifa
 1Pe 3:1 wavutwe bila neno kupitia *mwendo*
 1Pe 3:16 waabishwe kwa *mwendo* wenu mzuri

MWENENDO MPOTOVU, Gal 5:19 *mwendo mpotovu*
 2Pe 2:7 Loti aliyetaabishwa na *mwendo mpotovu*

MWENZEZA-INJILI, Mdo 21:8 Filipu *mwenzeza-injili*
 2Ti 4:5 fanya kazi ya *mwenzeza-injili*

MWENYE ENZI KUU, Zb 73:28 *Mwenye Enzi Kuu* kimbilio
 Mdo 4:24 *Mwenye Enzi Kuu* uliumba

MWEPESI, Yak 1:19 si *mwepesi* wa kusema

MWEREVU, Met 12:23 *mwererevu* hufunika mambo
 Met 14:15 *mwererevu* hutafakari kila hatua
 Met 22:3 *mwererevu* huona hatari na kujificha

MWEZI, Yoe 2:31 *mwezi* utatiwa damu
 Lu 21:25 ishara katika jua na *mwezi* na nyota

MWIBA, 2Ko 12:7 nilipea *mwiba* katika mwili
MWILI, Mwa 2:24 watakuwa *mwili* mmoja
 Ayu 33:25 *Mwili* wake na uwe na alya fukiko ujana
 Mt 10:28 msywaogope wale wanaoewa *mwili*
 Mt 26:26 Chukueni mle. Huu unamaanisha *mwili* wangu
 Ro 8:5 wanaoishi kulingana na *mwili* hukaza
 1Ko 7:4 hana mamlaka jua ya *mwili* wake, bali mke
 1Ko 12:18 Mungu amepanga kila kiungo cha *mwili*
 1Ko 15:44 Hupandwa ukiwa *mwili* wa nyama
 Gal 5:19 matendo ya *mwili* huonekana wazi
 Flp 3:21 atageuza *mwili* wetu wa hali ya chini

MWINDAJI, Zb 91:3 mtego wa *mwindaji* wa ndege

MWISHO, Isa 2:2 Katika siku za *mwisho*
 Mt 24:14 ndipo ule *mwisho* utakopokuja
 Yoh 13:1 Yesu aliwapenda wali wake mpaka *mwisho*
 2Ti 4:7 nimekimbia mbio mpaka *mwisho*

MWITO, Efe 4:1 mtembee kwa kustahili *mwito*

MWIZI, Met 6:30 *mwizi* akiiba anapokuwa na njaa
 Met 29:24 Rafiki ya *mwizi* hujichukia
 Mt 24:43 angejua *mwizi* atakuja kesho gani
 1Th 5:2 siku inakuja kama *mwizi* usiku

MWOKOZI, 2Sa 22:3 kimbilio langu, *mwokozi* wangu
 Mdo 5:31 alimwinua *Mwokozi* Mkuu na *Mwokozi*

MWONGO, Zb 101:7 *mwongo* hatasimama mbele yangu
 Met 19:22 afadhali kwa maskini kuliko *mwongo*
 Yoh 8:44 Ibilisi ni *mwongo*, baba ya uwongo

MWONGOZO, 1Nya 28:12 ramani kupitia *mwongozo* wa
MWOVU, Met 29:2 *mwovu* anapotawala, watu hulia
 Isa 26:10 *mwovu* akionyesha kibali, hatajifunza
 1Yo 5:19 ulimwengu katika nguvu za *mwovu*

MYAHUDI, Zek 8:23 watashika joho la *Myahudi*
 1Ko 9:20 Kwa *Wayahudi* nilikuwa kama *Myahudi*

MZABIBU, Mik 4:4 kila mtu chini ya *mzabibu* wake
 Yoh 15:1 Mimi ndiye *mzabibu* wa kweli

MZAHA, Mwa 19:14 Loti alionekana anafanya *mzaha*
 Met 26:19 Nilikuwa nikifanya *mzaha* tu

MZALIWA PEKKE, Yoh 1:18 mungu *mzaliwa pekee*
 Yoh 3:16 akamtua Mwana wake *mzaliwa pekee*

MZALIWA WA KWANZA, Zk 11:5 *mzaliwa wa kwanza*, Misi
 Koli 1:15 *mzaliwa wa kwanza* wa viembe vyote

MZEE WA SIKU, Da 7:9 *Mzee wa Siku* akaketi
MZEITUNI, Zb 52:8 *mzeituni* katika nyumba ya Mungu
 Ro 11:17 *mzeituni* wa mwituni, ulipandikizwa

MZEMBE, Met 19:15 mtu *mzembe* atakaa njaa
 Da 6:4 Danieli hakupatikana akiwa *mzembe*

MZIGO, Zb 38:4 dhambi zangu kama *mzigo* mzito
 Zb 55:22 Mtupia Yehova *mzigo* wako
 Zb 68:19 Yehova anatumbea *mzigo* kila siku
 Mdo 15:28 tusiwaogeeze ninyi *mzigo* zaidi ila
 Gal 6:5 kila mtu ataubeba *mzigo* wake
 1Th 2:6 tungeweza kuwa *mzigo* wenyne gharama
 Ufu 2:24 siwaogeezi *mzigo* mwingine wotote

MZIGO MZITO, 1Yo 5:3 amri zake si *mzigo* mzito

N

NABII, Kum 18:18 Nitawainulia *nabii* kama wewe
 Eze 2:5 watajua *nabii* alikuwa miongoni mwaoo
 Amo 7:14 sikuwa *nabii* wala mwana wa *nabii*

NADHIRI, Kum 23:21 Ukiweka *nadhiri* kwa Yehova
 Amu 11:30 Yeftha akaweka *nadhiri*

NAFAKA, Zb 72:16 Kutakuwa na *nafaka* nyingi duniani

NAFASI, Gal 6:10 tukiwa na *nafasi*, tutende mamba
NAFSI, Hes 31:28 *nafsi* moja ya watu na ya wanyama
 Eze 18:4 *Nafsi* inayotenda dhambi itakufa
 Mt 22:37 mpende Yehova kwa *nafsi* yote

NAFSI YOTE, Efe 6:6 tufanye kwa *nafsi* yote
 Kol 3:23 mnalofanya, lifanyeni kwa *nafsi* yote

NAINI, Lu 7:11 akasafiri kwenda jiji linaloitwa *Naini*

NAKALA, Kum 17:18 ajiandikie *nakala* ya Sheria hii

NANGA, Ebr 6:19 tumaini kama *nanga* ya *nafsi*

NATHANI, 2Sa 12:7 *Nathani* akamwambia Daudi: Wewe
NCHI, Isa 66:8 *nchi* itazaliwa katika siku moja?
NDAMA, Kut 32:4 akatengeza sanamu ya *ndama*
 Isa 11:6 *ndama* na simba watakuwa pamoja
NDANI, 2Ko 4:16 mtu tuliye kwa *ndani*
 Efe 3:16 kuwa na uwezo katika mtu miye kwa *ndani*

NDANI KABISA, Ufu 2:23 mawazo ya *ndani kabisa*

NDEGE, Mt 6:26 Waangalieni kwa makini *ndege*

NDIYO, Mt 5:37 'Ndiyo' yenu imaanishe *ndiyo*

NDOA, Mt 22:2 mfalme aliyeanzika karamu ya *ndoa*
 Yoh 2:1 karamu ya *ndoa* katika Kana
 1Ko 7:9 bora kufunga *ndoa* kuliko kuwaka tamaa
 1Ko 7:36 hafanyi dhambi. Acheni afunge *ndoa*
 1Ko 7:38 asiyefunga *ndoa* atafanya vema zaidi
 Ebr 13:4 *Ndoa* na iheshimiwe kati ya wote
 Ufu 19:7 *ndoa* ya Mwanakondoo imefika

NDOTO, Mhu 5:3 *ndoto* huja kwa sababu ya shughuli
NDUGU, Met 17:17 *ndugu* kwa ajili ya nyakati za taabu
 Met 18:24 anayeshikamana kwa ukaribu kuliko *ndugu*
 Mt 13:55 na *ndugu* zake Yakobo, Yosefu, na
 Mt 23:8 nanyi nyote ni *ndugu*

NDUGU, Mt 25:40 mliyovutendea *ndugu* yangu
 1Ko 5:11 anayeitwa *ndugu* ambaye ni
 1Pe 5:9 ushirika mzima wa *ndugu* zenu

NEBUKADNEZA, Da 2:1 *Nebukadnezar* aliota ndoto

NENO, Met 25:11 *neno* linalosema wakati unaofaa
 Isa 55:11 hakika *neno* langu litafanikiwa
 Lu 8:12 Ibilisi huliondoa ile *neno* miyoni
 Yoh 1:1 Hapo mwanzo *Neno* alikuwako
 Yoh 17:17 *neno* lako ni kweli
 Mdo 18:5 Paulo ashughulikia sana na *neno*
 Flp 2:16 kulishika sana *neno* la uzima
 2Ti 2:15 ukilitumia sawasawa *neno* la kweli

NENO LA MUNGU, Isa 40:8 *neno la Mungu* linadumu
 Mk 7:13 mnalibatisha *neno la Mungu* kwa mapokeo
 1Th 2:13 milikubali kama *neno la Mungu*
 Ebr 4:12 *neno la Mungu* liko hali nalo ni lenye nguvu
NG'AA, Isa 14:12 anguka kutoka mbinguni, unayeg'aa
NG'OMBE DUME, Kut 21:28 *Ng'ombe dume* akimpiga
 Kum 25:4 kumfunga kinywa *ng'ombe dume*
 Met 7:22 anamfuata kama *ng'ombe dume* machinjioni
 Ho 14:2 kutoa sifa kama *ng'ombe dume*
 1Ko 9:9 anahangaikia *ng'ombe dume*?

NGAMIA, Mt 19:24 ni rahisi zaidi kwa *ngamia* kupita
NGANO, Mt 13:25 kupanda magugu kati ya *ngano*
NGAO, Zb 84:11 Yehova Mungu ni jua na *ngao*
 Efe 6:16 chukueni *ngao* kubwa ya imani

NGAZI, Mwa 28:12 ngazi, kilele kufika mbinguni
NGOJEA, Zb 37:7 umngoeje Yehova kwa matumaini
NGOME, Zb 18:2 Yehova ni ngome yangu
 Isa 25:4 umekuwa ngome kwa maskini
 Lu 19:43 ngome yenye miti iliyochochoka
 2Ko 10:4 kuzipindua ngome zenye nguvu
NGUO, Yak 2:15 ndugu au dada hana nguo
NGURUWE, Lu 8:33 roho waovu wakawaingia nguruwe
 Lu 15:15 alimpeleka shambani akalisha nguruwe
 2Pe 2:22 nguruwe aliyeshwa amegaaga
NGUVU, Zb 29:11 atawapa nguvu wata wake
 Zb 31:10 Nguvu zinapungua, dhambi yangu
 Zb 84:7 kutembea kutoka nguvu hadi nguvu
 Met 17:22 roho iliyopondeka hufyonza nguvu
 Isa 35:4 Iweni na nguvu. Msiogope
 Isa 40:28 Yehova haishiwi na nguvu
 Isa 40:29 humpa nguvu mtu aliyechoka
 Isa 40:31 wanaotumaini Yehova watapata nguvu
 Isa 41:10 Nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia
 Zek 4:6 si kwa nguvu, bali kwa roho yangu
 Mk 5:30 akahisi nguvu zimetoka
 Mdo 12:30 mpende Yehova kwa nguvu zako zote
 Mdo 1:8 roho takatifu ikija mtapokea nguvu
 Ro 15:1 beba udhaifu wa wasio na nguvu
 1Ko 16:13 simameni imara, iweni na nguvu
 2Ko 4:7 nguvu zinazopita zile za kawaida
 2Ko 12:9 nguvu zangu zinakamilika katika udhaifu
 2Ko 12:10 ninapokuwa dhafi, ninakuwa na nguvu
 Flp 4:13 Kwa mambo yote nina nguvu
 Ufu 3:8 ninajua kwamba una nguvu kidogo
NGUZO, Mwa 19:26 mke wa Loti akawa nguzo ya chumvi
 Kut 13:22 nguzo ya wingu, nguzo ya moto
 Gal 2:9 walioonekana kuwa nguzo
 1Ti 3:15 nguzo na tegemezo la ile kweli
NIA, Met 16:2 Yehova huchunguza nia
NICHUNGUZE, Zb 26:2 *Nichunguze*, Ee Yehova
 Gal 6:4 kila mmoja na *achunguze* matendo yake
NIDHAMU, Met 1:7 wapumbua wanadharau *nidhamu*
 Met 3:11 usikatae *nidhamu* ya Yehova
 Met 19:18 Mtie *nidhamu* mtoto wako
 Met 23:13 Usimnyime mvulana *nidhamu*
 Ebr 12:11 *nidhamu* inayoonekana yenye shangwe
 Ufu 3:19 huwakaripia na kuwatia *nidhamu*
NINAWI, Yon 4:11 Je, sipaswi kuliuhurumia *Ninawi*?
NIRA, 1Fa 12:14 baba alifanya *nira* yenu kuwa nzito
 Mt 11:30 *nira* yangu ni laini
 2Ko 6:14 Msifungwe *nira* pamoja na wasio waamini
NITAKUWA, Kut 3:14 *Nitakuwa* amenituma kwenu
NJAA, Isa 65:13 watakula, ninyi mtakuwa na njaa
NJAA KALI, Zb 37:19 Wakati wa njaa *kali* watakua
 Amo 8:11 Si njaa *kali* ya chakula au kiu ya maji
NJE, 1Ko 5:13 Mungu akiwahukumu wale walio nje
 Kol 4:5 hekima kuelekea wale walio nje
NJIA, Met 16:25 njia inayoonekana kuwa sawa
 Isa 30:21 Hii ndiyo njia. Tembeni ndani yake
 Yoh 14:6 Mimi ndiye njia na kweli na uzima
 Mdo 9:2 wanamu na wanawake wa Ite Njia
 1Ko 4:17 Atawakumbusha njia zangu
 1Ko 10:13 atafanya pia njia ya kutokea
 Flp 1:27 Jijendesheni kwa njia inayotahili habari njema
NJIWA, Mt 3:16 roho ya Mungu ikishuka kama njywa
 Mt 10:16 wasio na hatia kama njywa
NJOONI, Isa 55:1 Njoooni, ninyi nyote mlio na kiu
 Ufu 22:17 yeyote anayesikia na aseme, Njoooni
NOA, Mwa 6:9 Noa alitembea pamoja na Mungu
 Mt 24:37 kama siku za Noa zilivyokuwa, ndivyo
NUNUA, 1Ko 7:23 *Mlinunuliwa* kwa bei
 Ufu 5:9 kwa damu yako ukamnunuka watu
NURU, Zb 36:9 Kwa *nuru* yako tunaona *nuru*
 Zb 119:105 Neno lako ni *nuru* ya njia yangu
 Met 4:18 kijia cha waadilifu ni *nuru* nyangavu
 Isa 42:6 kama *nuru* kwa mataifa
 Mt 5:14 Ninyi ndiyo *nuru* ya ulimwengu
 Mt 5:16 acheni *nuru* yenu inganze
 Yoh 8:12 Mimi ndiye *nuru* ya ulimwengu
 2Ko 4:6 *Nuru* na inganze kutoka katika giza
NYAKATI, Lu 21:24 *nyakati* zilizowekwa za mataifa

NYAMA, Met 23:20 wanaokula nyama kwa pupa
 1Ko 15:50 nyama na damu haviwezi kuirithi Ufalme
NYAMAZA, Zb 4:4 Zunguma moyoni, na *nyamazazi*
 Zb 32:3 *Niliponyamazazi*, mifupa yangu iliidhoofika
 Mhu 3:7 Wakati wa *kunyamazazi* na wa kuongea
NYAMAZISHA, 1Pe 2:15 *nyamazishi* maneno ya kijinga
NYANG'ANYA, Law 19:13 *Usimnyang'anya* mwenzako
NYARA, Kum 24:7 akiwa ametekela nyara lazima auawe
 Yer 39:18 Uhai wako utakuwa kama nyara
NYAVU, Lu 5:4 mshushie nyavu zenu, mvue samaki
NYEKUNDU, Isa 1:18 Ingawa dhambi zenu ni *nyekundu*
NYENYEKEA, Mt 18:4 atakayejiinyenyekeza kama mtoto
 Ebr 13:17 mnyenyekee wale wanaoongoza
NYENYEKEZA, Kum 8:2 ili awanyenyekeze na kuwajaribu
NYEPESI, 2Ko 4:17 dhiki ni ya muda na ni *nyepesi*
NYEUPE, Ufu 7:14 wamefua kanzu na kuzifanya *nyeupe*
NYIKA, Isa 35:6 maji yatabubujika *nyikani*
 Isa 41:18 Nitaigeza *nyika* kuwa dimbwi la maji
NYIMA, Zb 84:11 Yehova *hatawanyima* jambo jema
NYIMBO, Ne 12:46 *nyimbo* za kumsifu Mungu
 Kol 3:16 *nyimbo* za kiroho zinazoiomba
NYOKA, Mwa 3:4 nyoka akamwambia mwanamke
 Yoh 3:14 Musa alivyoinua nyoka *nyikani*
NYONYESHA, 1Th 2:7 kama noma anayenyonyesha
NYOTA, Zb 147:4 anaziita *nyota* zote kwa majina
 Mt 24:29 baada ya dhiki *nyota* zitaanguka
 Ufu 2:1 *nyota* saba kwene mkono wake
NYUMA, Lu 9:62 anayeshika jembe na kutazama *nyuma*
NYUMBA, Zsa 7:13 atakayejenga *nyumba* kwa ajili ya
 Zb 27:4 nikae katika *nyumba* ya Yehova sikuzote
 Zb 101:2 utimilifu ndani ya *nyumba* yangu
 Zb 127:1 Yehova asipojenga *nyumba*
 Isa 56:7 *nyumba* yangu itaitwa *nyumba* ya sala
 Isa 65:21 Watajenga *nyumba* na kuishi ndani yake
 Lu 2:49 ninapaswa kuwa katika *nyumba* ya Baba
 Yoh 2:16 kuifanya *nyumba* ya Baba yangu *nyumba* ya
 Yoh 14:2 Katika *nyumba* ya Baba mna makao mengi
 Mdo 5:42 na kufundisha *nyumba* kwa *nyumba*
 Mdo 7:48 Aliye Juu Zaidi haishi katika *nyumba*
 Mdo 20:20 hadharani na *nyumba* kwa *nyumba*
 2Ko 5:1 tutapata *nyumba* ya milele mbinguni
 Efe 2:19 washirikiki wa *nyumba* ya Mungu
 Ebr 3:4 kila *nyumba* hujengwa na mtu fulani
NYWELE, Mt 10:30 hata nywele zenu zimehasabiwa
 Lu 21:18 hakuna hata nywele wa vichwa vyenu
 1Ko 11:14 nywele ndetu ni abuu kwa mwanamume
NZIGE, Yoe 1:4 kilichoachwa na *nzige* wanaoruka

O

OA, Kum 7:3 Msioane nao kamwe
 Mt 22:30 katika ufufuo, *hawaoni* wala *kuolewa*
 Mt 24:38 kabla ya Gharika, *wakioa* na *kuolewa*
 1Ko 7:32 Mwanamume ambaye *hajaoa* huhangaikia
OGA, 2Fa 5:10 Nenda *ukaoga* mara saba, Yordani
OGOPA, 2Nya 20:15 *Msiogope* kwa sababu ya umati huu
 Zb 56:4 ninatumaini Mungu; *siogopi*
 Zb 118:6 Yehova yuko upande wangu; *sitaogopa*
 Isa 41:10 *Usiogope*, niko pamoja nawe
 Mik 4:4 hakuna yeyote atakayeogopesha
 Ufu 2:10 *Usiogope* mateso yatakatyokupata
OGOPESHA, Ebr 10:31 jambo lenye *kuogopesha*
OGOPESHWA, Flp 1:28 bila *kuogopesha* na wapinzani
OKOA, Isa 59:1 Mkonu si mfupi usiweze *kuokoa*
 Mt 16:25 anayetaka *kuuokoa* uhai wake
 Lu 19:10 Mwana wa binadamu alikuja *kuokoa*
 1Ti 4:16 *utajiokea* na wale wanaokusikiliza
OKOLEWA, Mt 24:22 hakuna mwili ambao *ungekolewa*
OLE, Isa 5:20 Ole wanaosema wema ni uovu
 1Ko 9:16 ole wangu nisipotangaza habari njema
 Ufu 12:12 Ole wa dunia na wa bahari
OLEWA, 1Ko 7:39 yuko huru *kuolewa*, katika Bwana
OMBA, Zb 2:8 *Niombe*, nitakupa mataifa
 Mt 6:8 anajua mnachohitaji kabla *hamjamwomba*
 Mt 7:7 Endeleeni *kuomba*, mtapewa
 Yoh 14:13 lolote *mtakaloomba* katika jina langu
 Ro 8:34 Kristo Yezu hutuomba
 2Ko 5:20 tunaomba Mpatanishwa na Mungu

Efe 3:20 kupita mambo yote *tunayoomba*
 1Yo 5:14 *tukiomba* kulingana na mapenzi yake
OMBOLEZA, Mt 5:4 Wenye furaha, *wanaoomboleza*
ONA, Mt 6:1 msionyeshe uadilifu ili watu *wawaone*
 Yoh 1:18 Hakuna ambaye *amemwona* Mungu
 Yoh 14:9 ambaye *amentiona*, *amemwona* Baba
ONDOA, 1Ko 5:13 *Mwondoezi* mwovu miongoni mweni
ONDOKA, 1Ko 7:15 asiyeamini akiwaua *kuondoka*
ONEA WIVU, Zb 37:1 *usiwaone* nyu watunda dhambi
 Zb 73:3 *niliwaone wivu* wene kiburi
ONEKANA, Ro 1:20 sifa zake *zisizoonekana*, *zinaonekana*
ONGOZA, Zb 48:14 Mungu *ataungoza* kwa umliele
 Yer 10:23 Mwanadamu hawezi *kuongoza* hatua yake
 Ebr 13:7, 17 wale *wanaongoza* kati yenu
 Ebr 13:7, 17 Watini wale *wanaongoza*
ONGOZWA, 2Ti 3:16 kila andiko *limeongozwa* na roho
ONJA, Zb 34:8 *Onjeni* mwone Yehova ni mwema
 Ebr 6:4 *wameonja* zawadi ya bure ya kimbingu
 1Pe 2:3 mradi tu *mmeonja*
ONYESHA, Lu 3:8 zaeni matunda *yanayoonyesha* toba
 Yoh 5:20 Baba *humwonyesha* Mwana anayofanya
ONYO, Eze 3:17 lazima uwape *onyo* langu
 Eze 33:4 asitii *onyo*, damu yake itakuwa
 1Ko 10:11 yaliandikwa ili kuwa *onyo* kwetu
OSHA, Zb 51:2 *Nioshe* kabisa kutoka katika kosa langu
 Yoh 13:5 akaanza *kuiosha* miguu ya wanafunzi
OSHWA, 1Ko 6:11 *mmeosha* mkwa safi, mmetakaswa
OYVOOYVO, Ayu 6:3 mazungumzo ya *oyvooyvo*
OZA, Efe 4:29 Neno *lililoza* lisitoke kinywani

P

PAJI, Eze 3:9 *paji* gumu kuliko jiwe gumu
PAMBANA, Efe 6:12 *tunapambana*, si dhidi ya damu
PAMBO, Da 11:45 milima mtakatifu wa ile *Pambo*
PANDA, Zb 126:5 *wanaopanda* mbegu kwa machozi
 Mhu 11:6 *Panda* mbegu zako asubuhi na
 Isa 65:22 Wala *hawatapanda* watu wengine wale
 Yoh 3:13 hakuna mtu *aliyepanda* mbinguni
 1Ko 3:6 *niliipanda*, Apolo akatia maji, Mungu akakuza
 Gal 6:7 *analopanda* mtu, ndilo atakalovuna
PANGA, Isa 2:4 *panga* zao ziw majembe
 Ro 13:14 msive *mkipanga* mapema kwa ajili ya
PANGO, Mt 21:13 kuwa *pango* la wanyaonyani
PANZI, Isa 40:22 wakaaji wake ni kama *panzi*
PAPASA-PAPASA, Mdo 17:27 *watapapasa-papasa*
PARADISO, Lu 23:43 utakuwa nami katika *Paradiso*
 2Ko 12:4 ambaye alinyakuliwa kuingia *paradiso*
PASAKA, Kut 12:11 Ni *Pasaka* ya Yehova
 Kut 12:27 Tunamtolea Yehova dhabihu ya *Pasaka*
 1Ko 5:7 Kristo mwanakondoo wetu wa *Pasaka*
PATAKATIFU, Kut 25:8 Mtanijenge mahali *patakatifu*
 Kut 26:33 *Patakatifu* na *Patakatifu* Zaidi
 Zb 73:17 Mpa *niliopingia patakatifu* pa Mungu
PATANA, 1Ko 7:11 au *apatane* tena na mume wake
PATANISHA, 2Ko 5:19 Mungu *alipatanisha* ulimwengu
PATANISHWA, Ro 5:10 *tulipatanisha* na Mungu
PAULO, Angalia SAULI, 1Ko 1:12 Mimi ni wa *Paulo*
PEKE YANGU, Yoh 16:32 mtianchika *peke yangu*
PEMBE, Da 7:7 mnyama wa nne alikuwa na *peembe* kumi
 Da 8:8 ile *peembe* kubwa ikavunjika
PENDA, Law 19:18 *umpende* mwenzako kama
 Kum 6:5 *umpende* Yehova kwa moyo wote
 Met 8:30 Mimi ndiye *aliyenipenda* sana
 Mt 10:37 Yeyote *anayependa*
 Mt 22:37 Lazima *umpende* Yehova Mungu wako kwa
 Mk 10:21 Yesu *akapenda* na kumwambia
 Yoh 3:16 Mungu *alipenda* ulimwengu sana
 Yoh 12:25 *anayependa* uhai wote huanamiza
 Yoh 13:1 *aliwapenda* walio wote mpaka mwisho
 Yoh 13:34 kwamba *mpendane*
 Yoh 14:15 *mnanipenda*, mtazishika amri zangu
 Yoh 21:17 Simoni, je, *unanipenda*?
 Ro 13:8 Msiwe na deni, isipokuwa *kupendana*
 1Ko 12:18 amepanga kila kuingo kama *aliyependa*
 Gal 2:20 Mwana wa Mungu, *aliyenipenda*
 Kol 3:19 waume, edeleeni *kuwapenda* wake zenu
 1Ti 6:4 *anapenda* sana kubishana
 1Yo 2:15 *Msiupende* ulimwengu au vitu vilivyoti

1Yo 3:18 *kupendana*, si kwa neno au kwa ulimi
 1Yo 4:10 si kwamba sisi *tumpendana* Mungu
 1Yo 4:20 ambaye *hampendi* ndugu, *hampendi* Mungu
 1Yo 5:3 *kumpenda* Mungu humanisha
 Ufu 3:19 *ninaowapenda*, mimi huwakaripia
PENDEKEZA, Ro 5:8 Mungu *hupendekeza* upendo
 2Ko 4:2 *tunajipendekeza* kwa kila dhambi
 2Ko 6:4 kwa kila njia *tunajipendekeza* kuwa
PENDELEA, Fup 10:17 Mungu *asiyempendelea* yeyote
PENDELEO, Kip 1:29 *pendeleo* kuteseka kwa ajili yake
PENDEZA, Zb 147:1 Jinsi *inayopendeza* kumsifu!
 Yoh 8:29 sikuzote mimi hufanya *yanayompendeza*
 Ro 15:1 tusiwe *tukijipendeza* wenyewe
 Ro 15:2 *ampendeze* jirani yake kwa mema
 Ro 15:3 hata Kristo *hakujipendeza* mwenyewe
 1Ko 10:33 ninavyojaribu *kuwapendeza* watu wote
 Gal 1:10 je, ninajaribu *kuwapendeza* wanadamu?
 1Ko 10:10 Kama *ninawapendeza* wanadamu
 Efe 6:6 ili tu *kuwapendeza* wanadamu
 Kol 1:10 ili *kumpendeza* kikamili Yehova
PENDEZWA, Zb 1:2 *anapendeza* na sheria ya Yehova
PENDWA, Yer 8:6 njia *inayopendwa* na wengi
PEPERUSHWA, Ebr 2:1 ili *tusipeperushwe* kampe
PEPO, Ufu 7:1 wakizishika *pepo* nne za dunia
PESA, Mhu 7:12 *pesa* ni ulinzi
 Mhu 10:19 *pesa* ni jawabu la mahitaji yote
 1Ti 6:10 *kupenda pesa* chanzo cha mabaya
 Ebr 13:5 bila upendo wa *pesa*
PETRO, Mt 14:29 *Petro* akatembea juu ya maji
 Lu 22:54 *Petro* alikuwa akiwafuata kwa mbali
 Yoh 18:10 *Petro* alikuwa na upanga
 Mdo 12:5 *Petro* alikuwa gerezeni lakini kutaniko
PEWA, Lu 12:48 *aliyepewa* mengi atadaiwa mengi
PICHA, Ro 2:20 una *picha* ya ujuzi na ya ile kweli
PIGA, 2Ko 6:5 kwa *kupigwa*, kufungwa gerezeni
PIGA HEWA, 1Ko 9:26 nisikimbie na *kupiga hewa*
PIGANA, 2Nya 20:17 Hamtahitaji *kupigana* vita hivi
 Mdo 5:39 huenda ikawa *mnapigana* na Mungu
 1Ti 6:12 *Pigana pigano* zuri la imani
 2Ti 2:24 mtumwa wa Bwana *hahitaji kupigana*
PIGANO, Yud 3 mfanye *pigano* kali kwa ajili ya imani
PIGAPIGA, 1Ko 9:27 *ninaupigapiga* mwili wangu
PIGO, Kut 11:1 Nitamletea Farao na Misri *pigo* moja zaidi
PILATO, Yoh 19:6 *Pilato*: Sijampata na kosa lolote
PIMA, Met 27:21 mtu *hupimwa* kwa sifa anayopokea
 Da 5:27 *umpimwa* na kuonekana umeponguika
PINDA, Mhu 1:15 *Kilichopinda* hakivezi kuniyoshwa
PINDUA, 2Ko 10:4 *kuzipindua* ngome zenye nguvu
PINGA, Mdo 17:7 wote *wanapiga* maagizo ya Kaisari
PITA, 1Ko 4:6 *Msipite* mambo yaliyoandikwa
POFUSHA, 2Ko 4:4 mungu wa mfumo huo *amezipofusha*
PONDEKA, Zb 34:18 Huwaokoa *waliopondeka* roho
 Met 18:14 kustahimili roho *iliyopondeka*
 Isa 42:3 *Hatapondeka* tete lililovunjika
 Isa 57:15 nainisha na wale *waliopondwa*
PONGEZA, 1Ko 11:2 *Ninawapongeza* kwa sababu
PONYA, 2Nya 36:16 hawangeweza *kuponywa*
 Zb 147:3 *Huwaponya* waliovunjika moyo
 Met 12:18 ulimi wa mwenye hekima *huponya*
 Lu 4:23 Daktari, *jiponye* mwenyewe
 Lu 9:11 *akawaponya* waliohitaji *kuponywa*
 Lu 10:9 *mponye* wagonjwa
 Mdo 5:16 wote *wakaponya*
 Ufu 22:2 majani yalikuwa ya *kuponya* mataifa
POOZA, Lu 5:24 akamwambia mtu *aliyepooza*: Simama
PORA, Ebr 10:34 makubali *kuporwa* mali zenu
POROJO, Met 20:19 anayependa *kupiga porojo*
 1Ti 5:13 wanapiga *porojo* na kujiingiza katika mambo
POTEA, Zb 119:176 tangatanga kama kondoo *aliyepotea*
 Eze 34:4 hamjawatafuta *waliopotea*
 Lu 15:24 alikuwa *amepotea* naye amepatikana
POTOSHA, Mt 24:24 *kuwapotosha* waliochaguliwa
POTOSHWA, Gal 6:7 *Msipotoshwe*: Mungu si
PRISILA, Mdo 18:26 *Prisila* na Akila wakamafanulia
PUMBABA, Yer 20:7 *Umenipumbaba*, Ee Yehova
PUMUA, Zb 150:6 Kila kitu *kinachopumua*, kimsifu Yah
PUMZI, Mwa 2:7 akampulizika *pumzi* ya uhai
PUMZIKA, Da 12:13 *Utapumzika*, lakini utisamama

PUNDA, Hes 22:28 Yehova akamfanya *punda* aongee

Zek 9:9 Mfalme wako amepanda *punda*

PUNJA, 1Ko 6:7 si afadhali mkubali *kupunjwa*

PUPA, Lu 12:15 mjilinde na kila aina ya *pupa*

1Ko 5:11 mwache kushirikiana na mtu mwenye *pupa*

1Ko 6:10 wenye *pupa* hawataarithi Ufalme wa Mungu

Kol 3:5 *pupa*, ambayo ni ibada ya sanamu

PUUZA, 1Th 4:8 *hampuuzi* mwanadamu, bali Mungu

1Ti 4:14 *Usipuuz*e zawadi uliyo nayo

R

RADI, Mt 24:27 *radi* inavyotokea mashariki na kuangaza

Lu 10:18 Shetani anguka toka mbinguni kama *radi*

RAFIKI, 2Nya 20:7 *rafiki* yako Abrahamu

Zb 55:13 *Rafiki* yangu mwenyewe ninayemjua

Met 17:17 *Rafiki* wa kweli hupenda nyakati zote

Met 18:24 *rafiki* anayeshikamana kuliko ndugu

Met 27:6 Majeraha yanayosababishwa na *rafiki*

Yoh 15:13 atoe uhai wake kwa ajili ya *rafiki* zake

Yoh 15:14 Ninini ni *rafiki* zangu ikiwa

Yak 2:23 Abrahamu akaitwa *rafiki* ya Yehova

RAHA, Lu 8:14 wanakengushwa na *raha* za maisha

RAHELI, Mwa 29:18 miaka saba nimpate *Raheli*

Yer 31:15 *Raheli* anawaliaa wanawe

RAMANI, Kut 26:30 hema la ibada kwa kufuata *ramani*

1Fa 6:38 nyumba kulingana na *ramani* yake

RARUA, Yoe 2:13 *Irarueni* mioyo yenu

REBEKA, Mwa 26:7 *Rebeka*, alikuwa mrembo

REFUSHA, Isa 54:2 *refusha* kamba za hema lak

REHANI, 2Ko 1:22 *rehani* ya kile kitakachokuja

Efe 1:14 *rehani* ya mapema ya urithi wetu

REHEMA, Kum 4:31 Yehova Mungu ni mwenye *reHEMA*

1Nya 21:13 kwa maana *reHEMA* zake ni nyingi

Ne 9:19 kwa *reHEMA* nyingi, hukuwaacha

Zb 78:38 Lakini alikuwa mwenye *reHEMA*

Met 28:13 anayeyaungama atawonyesha *reHEMA*

Isa 55:7 arudi kwa Yehova, atamwonyesha *reHEMA*

Met 5:7 Wenye furaha ni wenye *reHEMA*

Mt 9:13 Ninataka *reHEMA*, si dhahibu

Lu 6:36 muwe na *reHEMA*, kama Baba yenu

2Ko 1:3 Baba wa *reHEMA* nyororo

Yak 2:13 *ReHEMA* hushinda hukumu

Yak 5:11 Yehova, ana upendo mwororo na *reHEMA*

REKEBISHA, Kum 8:5 baba *anayemrekebisha* mwana

Zb 94:12 Mwenye furaha ni mtu *anayemrekebisha*

RIDHIKA, 1Ti 6:8 chakula na mavazi, *tutaridhika* na

RITHI, Mt 5:5 wapole *watairithi* dunia

Mt 25:34 *urithini* Ufalme uliotayarishwa kwa ajili yenu

ROHO, Hes 11:25 akachukua kiasi fulani cha *roho*

1Sa 16:13 *roho* ikaanza kumtia nguvu Daudi

2Sa 23:2 *Roho* ya Yehova ilisema kupitia mimi

Zb 51:10 uweke *roho* mpya ndani yangu

Zb 51:17 Dhahibu kwa Mungu, *roho* iliyovunjika

Zb 104:29 Ukiondoa *roho* yao, wanakufa

Zb 146:4 *Roho* hutoka, naye hurudi ardhini

Mhu 12:7 *roho* hurudi kwa Mungu

Isa 61:1 *Roho* ya Yehova iko juu yangu

Yoe 2:28 nitaiminima *roho* juu ya kila mwili

Zek 4:6 Si kwa jeshi, bali kwa *roho* yangu

Mt 3:16 *roho* ya Mungu ikishuka kama njira

Mt 12:31 anayekufuru *roho* takatifu hatasamehewa

Mt 26:41 *roho* inataka lakini mwili ni dhafu

Zb 23:46 naiweka *roho* yangu mikononi mwako

Yoh 4:24 Mungu ni *Roho*, wamwabudu kwa *roho*

Yoh 16:13 *roho* ya ile kweli, atawaongoza

Ro 8:16 *Roho* hutoa ushahidi na *roho* yetu

Ro 8:26 *roho* hutomba kwa kuugua

1Ko 15:44 hufufuliwa ukiwa mwili wa *roho*

2Ko 3:17 Yehova ni *Roho*

Gal 5:16 Endeeleni kutembea kwa *roho*

Gal 5:22 tunda la *roho* ni upendo

Gal 6:8 anayepanda kwa *roho*

Efe 6:12 tunapamba na majeshi ya *roho* waovu

1Pe 3:18 akafanywa kuwa hai katika *roho*

ROHO MWOVU, Mdo 16:16 *roho mwovu* wa uaguzi

ROHO TAKATIFU, Zb 51:11 usiondoolee *roho takatifu*

Lu 1:35 *Roho takatifu* uliufunika

Lu 3:22 *roho takatifu*, imbo kama la njwi

Lu 11:13 Baba huwapa *roho takatifu* wanaomwomba

Yoh 14:26 *roho takatifu*, itawafundisha mambo yote

Mdo 1:8 *roho takatifu* itakapokuja juu yenu

Mdo 2:4 wote wakajazwa *roho takatifu*

Mdo 5:32 Mungu amewapa *roho takatifu*

Efe 4:30 msiihuzunisho *roho takatifu* ya Mungu

ROHO WAOVU, Mt 8:28 waliokuwa na *roho waovu*

1Ko 10:20 huvitoe dhahibu kwa *roho waovu*

1Ko 10:21 mkishiriki meza ya *roho waovu*

Yak 2:19 *roho waovu* wanaamini na kutemeka

RUDI, Yoe 2:12 *rudini* kwangu kwa mioyo yenu yote

Mal 3:7 *Nirudieni*, nami nitawarudia

RUSHWA, Mhu 7:7 *rushwa* huopotoshwa moyo

Efe 4:14 watoe, tukirushwa kuwa na huku

S

SAA, Mt 24:36 Kuhusu siku hiyo na saa hiyo

SABABU, Isa 45:19 Nitafutei tu bila *sababu*

Ro 13:5 kuna *sababu* ya lazima kwenu kujitisha

SABATO, Kut 20:8 Ikumbuke siku ya *Sabato*

Mt 12:8 Mwana wa binadamu, Bwana wa *Sabato*

Mk 2:27 *Sabato* iliwekwa kwa ajili ya mwanadamu

Lu 14:5 Hatamtoa ng'ombe shimoni *Sabato*

Kol 2:16 yeyote asiwahukumu kuhusu *sabato*

Ebr 4:9 pumziko la *sabato* la

SAFI, Law 13:45 kusema, 'Mimi si *safi*, mimi si *safi!*'

Hab 1:13 Macho yako ni *safi* yasitazame uovu

Sef 3:9 nitabadilii lugha iwe lugha *safi*

Mt 5:8 Wenye furaha ni walio *safi* moyoni

Yoh 15:3 Tayarini nini *safi* kwa *sababu* ya neno

SAFINA, Mwa 6:14 Jitengezee *safina*

SAFISHA, Zb 51:2 *unisafishe* kutoka katika dhambi

Da 11:35 kazi ya *kuwasafisha* watu ifanywe

Da 12:10 Wengi *watasafisha*

Zek 13:9 *nitawasafisha* kama fedha *inavyosafisha*

2Ko 7:1 *tujisafishe* kila unajisi

SAHAU, Mku 4:23 Iwani waangalifu *msisahau*

Zb 119:141 *sijayasahau* maagizo yangu

Isa 49:15 mwanamke anaweka *kumsahau* mtoto?

Flp 3:13 *Ninayasahau* mambo ya nyuma

Ebr 6:10 Mungu hakosi kuwa *mwadilifu asahau*

SALA, Zb 65:2 Ee Msikaji wa *sala*

Zb 141:2 *Sala* itayarishwe kama uvumba

Met 15:8 *sala* ya wanyoofu humfurahisha

Met 28:9 *Duta sala* yake inachukiza

Ro 12:12 Humuni katika *sala*

2Th 3:1 endeeleni *kusali* kwa ajili yetu

Yak 5:15 *sala* ya imani itampoya huyo mgonjwa

1Pe 3:7 ili *sala* zenu zisizuwe

Ufu 8:4 uvumba ukapanda na *sala* za watakatifu

SALAMA, Met 12:3 Hakuna anayekuwa *salama* kwa uovu

SALI, 2Fa 19:15 Hezekia akaanza *kusali*

Da 6:13 *anasali* mara tatu kwa siku

Mt 5:44 *kusali* kwa ajili ya wale wanaowatesa

Mt 6:9 Basi, *salini* hivi:

Mk 1:35 Asubuhi na mapema, akaanza *kusali*

Mk 11:24 mambo yote *mnayosali* na kuomba

Lu 5:16 alienda mahali pasipo na watu ili *kusali*

Mdo 12:5 Petro gerezani, kutaniko *likisali*

Ro 8:26 hatujui kile tunachopaswa *kusali*

1Th 5:17 *Salini* bila kuacha

SALIMU, 2Yo 10 msimpokee nyumbani wala *kumsalimu*

SALITI, Mt 26:21 mmoja wenu *atanisali*

SAMAKI, Yon 1:17 akamtuma *samaki* ammeze Yona

Yoh 21:11 *samaki* wakubwa 153

SAMARIA, 2Fa 17:6 mfalme wa Ashuru ateka *Samaria*

SAMEHE, Ne 9:17 Mungu uliye tayari *kusamehe*

Zb 25:11 *Nisamehe* kosa langu, ingawa ni kubwa

Zb 103:3 *Husamehe* makosa yako yote

Met 17:9 *anayesamehe* kosa hutafuta upendo

Isa 55:7 Mungu *atasamehe* kwa njia kubwa

Mt 6:14 *mkiwasamehe* Baba yenu *atawasamehe* ninyi

Mt 18:21 *nimsamehe* mara ngapi? Saba?

Mt 26:28 itamwagui ili *wasamehe* dhambi

Kol 3:13 Kama Yehova *alivyowasamehe* kwa hiar

SAMSONI, Mdo 13:24 kumpa jina *Samsoni*

SAMWELI, 1Sa 1:20 Hana akamwita *Samweli*

1Sa 2:18 *Samweli* alikuwa akihudumu

SANAMU, Kut 20:4 Usijitengenezee *sanamu*
 Zb 11:5-4 *Sanamu* zao ni fedha na dhahabu
 Da 2:31 ulitazama na kuona *sanamu* kubwa sana
 Da 3:18 hatutaibudu *sanamu* ya dhahabu
 1Ko 6:9 waabudu-*sanamu* hawataurithi Ufalme
 1Ko 10:14 ikimbieni ibada ya *sanamu*
 1Yo 5:21 jipeshuni na *sanamu*

SANDUKU, Kut 25:10 *sanduku* la mshita
 2Sa 6:6 Uza akalikamata *Sanduku*
 1Inya 15:2 Hakuna anayepaswa kubeba *Sanduku*

SANHEDRINI, Mdo 5:41 wakatoka mbele ya *Sanhedrini*
SARA, Mat 17:19 Sara atakuzalima mwana
 1Pe 3:6 *Sara* alimiti Abrahamu, akimwita bwana

SAULI, 1Sa 15:11 Ninasikitika nimemwaka *Sauli* mfalme
 Mdo 7:58 miguuni pa kijana aliyetwa *Sauli*
 Mdo 8:3 *Sauli* akashambulia kutaniko
 Mdo 9:1 *Sauli* aliendelea kuwatisha wanafunzi
 Mdo 9:4 *Sauli*, *Sauli*, kwa nini unanitesa?

SAUMU, Hes 11:5 Tunakumbuka vitungu *saumu!*

SAUTI, 1Fa 19:12 Baada ya moto, *sauti* tulivu, ya chini
 Zb 19:4 *sauti* zake zimefika katika dunia yote
 Yoh 5:28 walio makaburini wataisika *sauti*
 Yoh 10:27 Kondoo wangu husilikiza *sauti* yangu

SAUTI YA CHINI, Yos 1:8 soma *Sheria* kwa *sauti* ya chini
 Zb 1:2 huifoma *sheria* Yake kwa *sauti* ya chini

SAYUNI, Zb 2:6 nimemwaka mfalme wangu *Sayuni*
 Zb 48:2 Miima *Sayuni*, jiji la Mfalme Mkuu
 Isa 66:8 *Sayuni* alizaa wana
 Ufu 14:1 Mwanakondoo juu ya Miima *Sayuni*

SEDEKIA, Yer 52:11 akampofusha macho *Sedekia*

SEHEMU YA KUMI, Ne 10:38 Walawi, *sehemu* ya kumi
 Mal 3:10 Leteni *sehemu* yote ya kumi

SENAKERIBU, 2Fa 19:16 maneno ambayo *Senakeribu*
SEREMALA, Mk 6:3 *seremala* mwana wa Maria

SHAHIDI, Ufu 1:5 Yesu Kristo, *Shahidi* Mwaminifu

SHAKA, Mt 21:21 mkiwa na imani nanyi msiwane na *shaka*
 Yak 1:6 kuomba kwa imani, bila *shaka*
 Yud 22 rehemu kwa wale walio na *shaka*

SHAMBA, Mt 13:38 *shamba* ni ulimwengu
 1Ko 3:9 Ninyi ni *shamba* la Mungu

SHAMBA LA MIZABIBU, Mt 20:1 *shamba* la *mizabibu*
 Mt 21:28 fanya kazi katika *shamba* la *mizabibu*
 Lu 20:9 alipanda *shamba* la *mizabibu* akasafiri

SHANGAA, 1Pe 4:4 *Wanashangaa* hamwendelei

SHANGILIA, 1Inya 29:9 *walishangilia* kwa kutoa matoleo
 Zb 100:2 Mtuikieni Yehova kwa *kushangilia*
 Zb 137:6 Sababu zangu kuu zaidi za *kushangilia*
 Met 8:30 *Ninashangilia* mbele zake wakati wote
 Met 27:11 Uwe na hekima, moyo wangu *ushangilie*
 Mhu 8:15 bora kuliko kula na kunywa na *kushangilia*
 Isa 65:13 Watumishi wangu *watashangilia*, lakini
 Mdo 5:41 wakatoka mbele ya *Sanhedrini*, *wakishangilia*
 Ro 5:3 *tushangilie* tukiwa katika dhiki
 Ro 12:12 *Shangilieni* katika tumaini
 Ro 12:15 *Shangilieni* na wale wanao*shangilia*
 Flp 3:1 endeeleni *kushangilia* katika Bwana
 Flp 4:4 *Shangilieni* sikuzote katika Bwana

SHANGWE, Ne 8:10 *shangwe* ya Yehova ngome yenu
 Ayu 38:7 Nyota za asubuhi *zilishangilia*
 Isa 65:14 Watumishi watapiga vigelegele kwa *shangwe*
 Lu 8:13 hulipokea neno kwa *shangwe*
 Lu 15:7 *shangwe* mbinguni mtenda dhambi akitubu
 Yoh 16:22 hakuna atakayeondoa *shangwe* yenu
 Ro 15:13 Mungu awajaze *shangwe* na amani
 1Th 1:6 kwa *shangwe* ya roho takatifu
 Ebr 12:2 *shangwe* iliyowekwa mbele yake, alivumilia
 3Yo 4 *shangwe* watoto wanatembera katika kweli

SHAURIANA, Met 15:22 huvunjika *wajoshauriana*

SHAVU, Mt 5:39 anayekupiga kofi kwenye *shavu* la kulia

SHAWISHI, 1Ko 2:4 maneno yene *kushawishi* ya hekima
 2Ko 5:11 tunaendelea *kuwashawishi* watu
 2Ti 3:14 uliyojifunza na *uliyoshawishiwa* kuamini

SHEOLI, Angalia **KABURI**.

SHEREHE, Law 23:4 Hizi ndizo *sherehe* za Yehova za

SHERIA, Zb 19:7 *Sheria* ya Yehova ni kamilifu
 Zb 40:8 *sheria* yako imo ndani yangu
 Zb 94:20 kinatunga matatizo kwa kutumia *sheria*

Zb 119:97 Jinsi ninavyoipenda *sheria* yako
 Yer 31:33 Nitaitia *sheria* yangu ndani yao
 Hab 1:4 *sheria* haifanyi kazi, na haki
 Ro 7:22 naipenda *sheria* ya Mungu
 Ro 10:4 *Sheria* Kristo ndiye mwisho wa *Sheria*
 Ro 13:8 anayempenda mwenzake ametimiza *sheria*
 Gal 3:24 *Sheria* mtunzaji ikitungoza kwa Kristo
 Gal 6:2 mtaitimiza *sheria* ya Kristo
 2Ti 2:5 shindana kulingana na *sheria*
 Yak 2:8 mnaifuata ile *sheria* ya kifalme

SHERIA YA MUNGU, Ro 7:22 naipenda *sheria* ya Mungu

SHETANI, Ayu 1:6 *Shetani* pia akaingia kati yao
 Zek 3:2 Yehova na akukemea, *Shetani*
 Mt 4:10 Nenda zako, *Shetani!* Imeandikwa
 Mt 16:23 Petro: "Nenda nyuma yangu, *Shetani!*
 Mk 4:15 *Shetani* huja na kuliondoa neno
 Ro 16:20 Mungu atampanda *Shetani* chini ya miguu
 1Ko 5:5 mumkabidhi mtu huyo kwa *Shetani*
 2Ko 2:11 ili *Shetani* asitushinde akili
 2Ko 11:14 *Shetani* hujifanya malaika wa nuru
 2Th 2:9 kupitia kazi ya *Shetani*
 Ufu 12:9 nyoka anayeitwa Iblisi na *Shetani*
 Ufu 20:2 *Shetani* kufungwa miaka 1,000

SHIDA, 1Pe 4:18 mwadilifu anaokolewa kwa *shida*

SHIKA, Mt 28:20 kuwafundisha *kushika* mambo yote
 Yoh 14:15 mkinipenda, *matashika* amri zangu
 Flp 2:16 *kulishika* sana neno la uzima

SHIKAMANA, Mwa 2:24 atashikamana na mke
 Kum 10:20 mnapaswa *kushikamana* na Yehova
 Yos 23:8 mnapaswa *kushikamana* na Yehova
 Lu 22:28 *mmeshikamana* nami katika majaribu
 Ro 12:9 *shikamaneni* na mema

SHILO, Mwa 49:10 mpaka *Shilo* atakapokuja

SHIMO, Met 26:27 Anayechimba *shimo* ataanguka ndani
 Da 6:7 kutupwa ndani ya *shimo* la simba
 Mt 15:14 kipofu, watatumbukia ndani ya *shimo*

SHIMO REFU, Ufu 11:7 mnyama kutoka *shimo* refu
 Ufu 17:8 Mnyama atapanda kutoka katika *shimo* refu
 Ufu 20:3 akamtupa katika *shimo* refu

SHINDA, Yer 1:19 watapigana nawe, *hawatakuhinda*
 Yoh 16:33 jipeni moyo! *nimeushinda* ulimwengu
 Ro 12:12 endelea *kuushinda* uovu kwa wema
 Ufu 2:7 atakayeshinda nitampa ruhusa ya
 Ufu 6:2 *akishinda* na kukamilisha ushindi wake

SHIRIKIANA, 1Ko 5:9 mwache *kushirikiana* na waasherati
 1Ko 15:33 *Kushirikiana* na wabaya huharibu
 2Th 3:14 mwache *kushirikiana* naye

SHIRIKINI, Ro 12:13 *Shirikini* kulingana na mahitaji yao

SHORE, Mt 10:29 *Shore* wawili huuzwa kwa sarafu

SHTAKA, Ro 8:33 Ni nani atakayewashitaki
 1Ti 5:19 Usikubali *mashtaka* dhidi ya mzee
 Tit 1:7 Mwanagalizi hapaswi kuwa na *shtaka*

SHTUA, Yoh 6:60 Maneno hayo *yanashtua*; nani
SHUGHULIKA, 1Th 4:11 *kushughulika* na mambo yenu
SHUJAA, Yer 20:11 Yehova pamoja nami kama *shujaa*

SHUKA MOYO, 1Th 5:14 wafarjini wale *waliochuka moyo*

SHUKRANI, Zb 95:2 Twendeni tukiwa na *shukrani*
 Met 29:21 akibembelezwa hatakuwa na *shukrani*
 Efe 5:20 mkimtolea *shukrani* Mungu
 Kol 3:15 mjonyeshe kuwa wenye *shukrani*

SHUKURU, Mt 5:21 vema *kukushukuru*, Ee Yehova
 Yoh 11:41 Baba, *ninakushukuru* umeniskia
 Mdo 28:15 alipowaoona, *akamshukuru* Mungu
 1Ko 1:4 Sikuzote *ninamshukuru* Mungu
 1Ti 1:12 *Ninamshukuru* Kristo Yesu

SHULE, Yoh 7:15 ingawa hafanuidisha *shuleni*

SHUTUMU, Mt 5:11 watu wanapowashutumua

SIFA, Met 27:21 mtu hupimwa kwa *sifa* anayopokea

SIFA ZA KUSTAHILI, Gal 6:1 *sifa* za *kustahili* kiroho

SIFU, 1Inya 16:25 Yehova ni mkuu na anastahili *kusifiwa*
 Zb 147:1 inavyopendeza na inavyofaa *kumsifu*
 Met 27:2 Acha mtu mwingine *akusifu*

SIFUSIFU, Met 26:28 kinywa *kinachosifu* huleta
 Met 29:5 anayemsifusifu jirani anautandaza wawu
 Ro 16:18 maneno ya *kusifusifu* wao huishawishi
 Yud 16 *wakiwasifusifu* ili wapate faida

SIHI, Ro 12:1 *ninawasilhi* kwa huruma
 Flm 9 *nikusilhi* kwa msingi wa upendo

SIKIA, Ro 10:14 *watasikiaje* bila mtu wa kuhubiri
Yak 1:19 mwepezi *kusikia*, si kusema

SIKILIZA, Met 1:5 mwenye hekima *msikiliza*
Eze 2:7 uwaambia, iwe *watasikiliza* au la
Mt 17:5 Mwanangu, mpendwa. *Msikilizeni*
Lu 10:16 Yeyote anayewasikiliza ananisikiliza
Mdo 4:19 *kuwasikiliza* ninyi badala ya Mungu

SIKITIKA, Mt 9:36 Alipoona umati *akausikitika*
Mt 20:34 Yesu *akawasikitika*, akagusa macho yao

SIKITIKIA, Ebr 4:15 *kuusikitika* udhaifu wetu

SIKITIKIWA, 1Ko 15:19 sisi ndio wa *kusikitikiwa*
Zb 84:10 *siku* moja katika nyua zako ni bora
Eze 4:6 *siku* moja kwa mwaka mmoja
Mt 24:36 Kuhusu *siku* hiyo na saa hiyo
2Pe 3:8 *siku* moja ni kama miaka elfu

SIKUKUU, Mwa 40:20 *sikukuu* ya kuzaliwa, Farao
Mt 14:6 *sikukuu* ya kuzaliwa, Herode

SIKU YA YEHOWA, Yoe 2:1 *siku* ya Yehova inakuja!
Ayo 5:18 *siku* ya Yehova itamaanisha nini kwenu?
Sef 1:14 *siku* ya Yehova iko karibu!
1Th 5:2 *siku* ya Yehova inakua kama mwizi
2Th 2:2 *siku* ya Yehova imefika
Zb 3:12 kuweka akilini *siku* ya Yehova

SIKU ZA MWISHO, 2Ti 3:1 *siku* za mwisho, hatari
SILAHA, Isa 54:17 Hakuna *silaha* yoyote itakayotokeza
2Ko 10:4 *silaha* za vita vyetu si za kimwili

SIMAMA, 1Ko 10:12 anayefikiri *amesimama* ajihadhari
SIMAMA IMARA, 1Ko 16:13 *simameni imara* katika imani

SIMAMIA, Ro 12:8 anayesimamia, na afanye hivyo kwa
1Th 5:12 wanaoasimamia katika Bwana

SIMBA, 1Sa 17:36 nilimua *simba* na dubu
Isa 11:7 *Simba* atakula majani kama ng'ombe
Da 6:27 alimwoka Danieli kutoka kwa *simba*
1Pe 5:8 Ibilisi, kama *simba* anayenguruma
Ufu 5:5 *Simba* wa kabila la Yuda

SIMONI, Mdo 8:18 *Simoni* akawatolea pesa
SINAI, Kut 19:20 Yehova akahuka, Milima *Sinai*
SINZIA, Met 23:21 *kusinzia* kutamvika matambara

SIRI, Zb 9b:1 mahali pa *siri* pa Aliye Juu Zaidi
Met 11:13 mtu anayeamnika hutunza *siri*
Met 20:19 Mchongezi hufunua mazungumzo ya *siri*
Met 25:9 usifunue uliyoambiwa *siri*
Ayo 3:7 kuwafunulia watumishi wake manabii *siri* yake
Flp 4:12 inayefunua *siri* ya jinsi ya kushiba

SIRI TAKATIFU, Ro 16:25 *siri takatifu* ilikuwa imefichwa
Efe 3:4 ninavyoelewa *siri takatifu*

SITASITA, Yak 1:8 yeye ni mtu *anayesitasita*, asiye imara

SODOMA, Mwa 19:24 kiberiti na moto juu ya *Sodoma*
2Pe 2:6 kuharibu *Sodoma*, kielelezo kwetu

SODOMA NA GOMORA, Yud 7 *Sodoma na Gomora*, onyo

SOKONI, Mdo 17:17 akajadiliana na watu *sokoni*

SOMA, Kum 17:19 *akisome* sikuzote za maisha yake
Mdo 8:30 kweli unajua *unayosoma*?

SONGA, Mk 4:19 *kulisonga* neno, nalo halizai matunda

STADI, Met 22:29 umemwona mtu aliye stadi katika kazi

STAHILI, Mt 10:11 tafuteni humo mtu *anayestahili*
2Ko 3:5 *kustahili* kwetu hutoka kwa Mungu
2Ti 2:2 *watastahili* kuwafundisha wengine

STAREHE, Lu 12:19 *starehe*, ule, unywe, na ujifurahishe

SUBIRA, Ne 9:30 Uliwaonyesha *subira* kwa miaka mingi
Met 14:29 asiye na *subira* hudhirihsia upumbavu
Met 25:15 Kwa *subira* kamanda hushawishiwa
Ro 9:22 Mungu alimuilima kwa *subira* vyombo
1Ko 13:4 Upendo ni wenyewe *subira* na fadhili
1Th 5:14 iweni na *subira* kwa watu wote
Yak 5:8 iweni na *subira*; imarisheni moyo yenu
2Pe 3:9 Yehova ni mwenye *subira* kwenu
2Pe 3:15 ioneni *subira* ya Bwana kwa wokovu

SUKUMA, Kut 35:21 moyo wake *ulimsukuma* akaleta

SULEMANI, 1Fa 4:29 Mungu akampa *Sulemani* hekima
Mt 6:29 hata *Sulemani* katika utukufu wake wote

SURA, 1Sa 16:7 Usitazame *sura* yake
Yoh 7:24 kuhukumu kwa *sura* ya nje

SURA NZURI, Met 31:30 *Sura nzuri* inaweza kundanganya

SURA YA NJE, Mt 22:16 huangali *sura* ya nje ya mtu
Gal 2:6 Mungu haangali *sura* ya nje

SWILA, Isa 11:8 atacheza juu ya shimo la *swila*

T

TAA, Zb 119:105 Neno lako ni *taa* ya mguu wangu
Mt 6:22 *Taa* ya mwili ni jicho
Mt 25:1 mabakira kumi waliochukua *taa* zao

TAABU, 2Sa 22:7 Katika *taabu* yangu nilimwita Yehova
Zb 46:1 Msaada unaopatikana nyakati za *taabu*
Isa 38:14 Ee Yehova, *ninataabika* sana

TABIBU. Angalia **DAKTARI**.

TAFADHALI, Mwa 15:5 *Tafadhali*, tazama juu mbinguni

TAFAKARI, Mwa 24:63 Isaka alikuwa *akitafakari*
Zb 19:14 *kutafakari* kwa moyo wangu
Zb 77:12 *Nitaufakari* utendaji wako wote
Met 15:28 mwadilifu *hutafakari* kabla ya kujibu

TAFUTA, 1Nya 28:9 *Ukintafuta*, atakuruhusu umpate
Zb 119:176 kondoo aliyepotea. *Nitafute* mimi
Isa 55:6 *Mtafuteni* Yehova wakati anapatikana
Eze 34:11 *nitawatafuta* kondoo wangu
Sef 2:3 *Mtafuteni* Yehova, ninyi wapole
Lu 15:8 afagie nyumba yake na *kuitafuta*
Yoh 4:23 Baba *anawatafuta* watu wa namna hiyo
Mdo 17:27 ili *wamtafute* Mungu
Kol 3:1 endeleeni *kutafuta* mambo yaliyo juu
1Pe 1:10 walifanya uchunguzi na *kutafuta*

TAI, Isa 40:31 Watapaa juu kwa mabawa kama *tai*
TAIFA, Kut 19:6 ufalme wa makuhani na *taifa* takatifu
Zb 33:12 furaha ni *taifa* ambalo Mungu ni Yehova
Isa 66:8 je, *taifa* litazaliwa mara moja?
Mt 21:43 Ufalme utapewa *taifa* linalozaa matunda
Mt 24:7 *taifa* litapigana na *taifa*
Mdo 17:26 kila *taifa* kutoka kwa mtu mmoja
1Pe 2:9 jamii iliyoachaguliwa, *taifa* takatifu

TAJA, Efe 5:3 *visitajwe* kamwe miongoni mwenu

TAJI, Met 12:4 Mke mwema ni taji kwa mume wake
Mt 27:29 wakasokota *taji* la miji
1Ko 9:25 hushindana wapat *taji* linaloharibika

TAJIRI, Yer 9:23 *tajiri* asijigambe kwa sababu ya utajiri
Ufu 3:17 unasema: Mimi ni *tajiri*

TAJIRISHA, Met 10:22 Baraka ya Yehova *hutajirisha*
2Ko 6:10 maskini lakini wanao*wtajirisha* wengi

TAKA, Kum 10:12 Yehova anataka mfanyo nini?
Mik 6:8 Yehova anataka nini kutoka kwako?

TAKASA, 1Fa 9:3 *Nimeitakasa* nyumba hii
Yer 1:5 kabla hujazaliwa *niikutakasa*
Eze 36:23 *nitalitakasa* jina langu kuu
Lu 11:2 Baba, jina lakina na litakaswe

TAKATAKA, 1Ko 4:13 kama *takataka* ya ulimwengu
Flp 3:8 ninavionga kuwa *takataka* nyingi

TAKATIFU, Law 19:27 Mnapaswa kuwa *watakatifu*
1Pe 1:15 iweni *watakatifu* katika mwenendo wenu

TALAKA, Mal 2:16 ninachukua *talaka*
Mt 19:9 *anayentaliki* mke wake isipokuwa kwa
Mk 10:11 *anayentaliki* mke wake na kumwoa mwingine

TALANTA, Mt 25:15 Akampa mmoja *talanta* tano

TAMAA, Zb 37:4 atatosheleza *tamaa* za moyo wako
Efe 2:3 kupatana na *tamaa* za mwili wetu
2Ti 2:22 zikimbie *tamaa* za ujana
Yak 1:14 hushawishiwa na *tamaa* yake
1Pe 2:11 mwendelee kujiepisha na *tamaa* za mwili
1Yo 2:16 *tamaa* ya mwili na *tamaa* ya macho

TAMANI, Kut 20:17 *Usimtamani* mke wa jirani yako
Ayu 14:15 *Utaitamani* kazi ya mikonjo yako
Zb 84:2 nafsi *inatamani* nyua za Yehova
Zb 84:2 nafsi yangu yote *inatamani* Yehova
Zb 145:16 kutosheleza *tamaa* ya kila kilicho hai
Isa 26:9 *ninakutamani* kwa nafsi yangu yote
Ro 1:15 *nitamtamani* kuwatangazia habari njema
Ro 7:18 nina *tamaa* ya kufanya mema lakini
Gal 5:16 hamtatenda kwa *tamaa* za mwili
Flp 1:8 *ninavyotamani* kuwaona ninyi

TAMASHA, 1Ko 4:9 tumekuwa *tamasha* kwa ulimwengu
1Ko 7:31 *tamasha* ya ulimwengu inabadilika

TAMBARARE, Zb 26:12 Mguu mahali *tambarare*

TAMBUA, 1Ko 16:18 *watambueni* watu wa namna hiyo

TAMBULIWA, 2Ko 6:9 wasiojulikana, *tunatambuliwa*

TANGATANGA, Zb 119:176 *Nimetangatanga* kama kondoo
Isa 53:6 *tumetangatanga* kama kondoo

TANGAZA, 1Ko 11:26 *kukitangaza* kifo cha Bwana

TANGAZO, Ro 10:10 *tangazo* la hadharani ili apate
Ebr 10:23 tushike imara *tangazo* la hadharani la
TANGI, Met 5:15 Kunywa maji ya *tangi* kila mwenyewe
TANURU, Da 3:17 Mungu atatuokoa kutoka katika *tanuru*
TARAJIWA, Mhu 9:11 matukio *yasiyotarajiwa* huwapata
TARSHISHI, Yon 1:3 Yona akainuka kwenda *Tarshishi*
TARTARO, 2Pe 2:4 aliwatupa malaika ndani ya *Tartaro*
TARUMBETA, 1Ko 14:8 *tarumbeta* ikipiga mwito
TASA, Kut 23:26 Hakuna mwanamke atakayekuwa *tasa*
Isa 54:1 Piga vigelegele, mwanamke *tasa*
TATU, Kum 16:16 Mara *tatu* kila mwaka, wanaume wote
TAWALA, Mwa 1:28 *mtawale* kila kiumbe aliye hai
Mwa 3:16 mume wako *atakatwala*
Zb 119:133 Jambo lolote ovu *lisinitawale*
Met 29:2 mwovu *anapotawala*, watu hulika
Mhu 8:9 mwanadamu *amemtawala* mwenzake
Ro 6:12 msiruhusu dhambi *itawale* kama mfalme
1Ko 6:12 sitaruhusu kitu chochote *kinitawale*
Ufu 11:15 *atawala* akwika mfalme milele na milele
TAWI, Yoh 15:4 tawi haliiwezi kuzaa likiwa peke yake
TAYARI, Mt 24:44 iweni *tayari*
Efe 6:15 *tayari* kutangaza habari njema
TAYARISHIA, Yoh 14:2 ninaenda *kuwatayarishia* mahali
TAZAMA, Kol 3:22 si wakati tu *wanapowatazama*
TAZAMIA, Mt 24:44 atakuja saa *msiyotazamia*
TEGEMEA, Met 3:5 *usitagemee* ulelewaji wako mwenyewe
Ro 12:18 kwa kadiri *inavyotagemea* ninyi
2Ko 1:9 *tusijitagemee*, *tumtagemee* Mungu
1Pe 4:11 *anayetagemee* nguvu ambazo Mungu hutoa
TEGEMEKA, Kut 18:21 wanaume *wanaotegemeka*
Zb 19:7 Kikumbusho cha Yehova *kinategemeka*
Zb 33:4 jambo analofanya Yehova *linategemeka*
TEKA, 2Ko 10:5 *tunaiteka* kila fikira
TEMBELEA, Mdo 15:36 *tukawatembelee* akina ndugu
TEMEA MATE, Mt 26:67 *wakamtemea mate* usoni
TENDA, Ayu 31:34 kuogopa umati *utakavyotenda*
TENGA, Ro 8:39 *kututenga* na upendo wa Mungu
TENGANISHA, Met 17:9 *huwatenganisha* marafiki
Mt 25:32 *atatenganisha* kama mchungaji
TESA, Zb 119:86 *Watu wananitesa* bila sababu
Mt 5:10 Wenye furaha ni wale *wamateswa*
Yoh 15:20 kiwa *wamenitesa*, *watawatesa* ninyi pia
Mdo 22:4 *Niliitesa* Njia hii kufika kifo
Ro 12:14 Endeleeni kuwabariki wale *wanaowatesa*
1Ko 4:12 *tunapoteswa*, tunavumilika bila subira
2Ko 4:9 *tunateswa*, lakini hatuachiwi bila msaada
TESEKA, Ayu 36:15 huwaokoa *wanaoteseka*
Ro 8:17 warithi mradi *tunateseka*
Flp 1:29 pendeleo *mteseke* kwa ajili yake
1Pe 3:14 *mkiteseke* kwa ajili ya uadilifu
TESWA, Zb 119:71 Ni vema kwamba *nimeteswa*
TETEFA, Flp 1:7 *kuitetea* na kuthibitisha kisheria
TETEMEKA, Flp 2:12 wokovu kwa *kutetemeka*
TETEMEKO, Lu 21:11 *matetemeko* makubwa ya ardhi
THAMANI, Met 3:9 Mheshimu kwa vitu vyenye *thamani*
Da 9:23 wewe ni mtu mwenye *thamani* sana
Hag 2:7 vitu vyenye *thamani* vitaingia
Mt 6:26 Je, ninyi si wenye *thamani* kuliko wao?
2Ko 10:7 kulingana na *thamani* yake ya nje
1Pe 1:19 kwa damu yenye *thamani*, ya Kristo
THAWABISHA, Ru 2:12 Yehova na *akuthawabisha*
THAWABU, Kol 3:24 *thawabu* kutoka kwa Yehova
THELUJI, Isa 1:18 dhambi kwia nyupeu kama *theluji*
THIBITISHA KISHERIA, Flp 1:7 *kuthibitisha kisheria*
TIA MAFUTA, 1Sa 16:13 Samweli *alimtia mafuta* Daudi
Zb 2:2 Wafalme dhidi ya *tiwa-mafuta*
Zb 105:15 Msiwaguse *watiwa-mafuta* wangu
Isa 61:1 Yehova *alinitia mafuta* nitangaze habari njema
TIA MOYO, 1Ko 14:31 wajifunze na *watiwe moyo*
TILI, Kut 24:7 tukyo *tayari* kuyafanya, nasi *tutatili*
1Sa 15:22 *Kutii* ni bora kuliko dhahibu
Zb 51:12 Chochea ndani yangu utayari wa *kukutii*
Yoh 3:36 *asiyemtii* Mwana hataona uzima
Mdo 5:29 Lazima *tumtii* Mungu kwa mtawala badala
Ro 5:19 kupitia *kutii* kwa mtu mmoja wengi
Ro 16:26 kuendeleza uti kwa imani
Efe 6:5 watumwa, *watini* mabwana wenu

Ebr 5:8 alijifunza *kutii* kutokana na mateso
Ebr 13:17 *Watini* wale wanaoongoza kati yenu
TISHA, 1Ko 15:27 *alivitiisha* vitu vyote chini yake
TIKISA, Hag 2:7 *nitayatikisa* mataifa yote
1Th 3:3 yeyote *asitikiswe* na dhiki hizo
2Th 2:2 *msitikiswe* upesi kwenye kufikiri kwenu
TIMIZA, Mt 5:17 Sikuja kuharibu, bali *kutimiza*
TIMOTHEO, Mdo 16:1 mwanafunzi aliyeitwa *Timotheo*
1Ko 4:17 namtuma *Timotheo*, mtoto mpendwa
1Ti 1:2 *Timotheo*, mwanangu halisi
TISHA, Mdo 4:17 bila *tuwatishwe* wasihubiri
Efe 6:9 njia hiyohiyohi, bila *kuwatisha*
TISHO, Met 3:25 Hutaogopa *tisho* la ghafila
TOA, Ro 6:13 *toeni* miili yenu kwa Mungu
TOA HESABU, Ro 14:12 kila mmoja wetu *atatoa hesabu*
1Ko 13:5 Hauweki *hesabu* ya ubaya
TOBA, Mdo 26:20 fanya matendo yanayoonyesha *toba*
Ro 2:4 Mungu anakuongoza kwenye *toba*
2Ko 7:10 huzuni ya kimungu hutokeza *toba*
TOFAUTI, Lu 11:47 *kutofautisha* viumbe walio safi na
Mal 3:18 mtaona *tofauti* kati ya mtu mwaadilifu na
TOFAUTISHA, Ebr 5:14 *kutofautisha* waliyo sawa na
TOHARA, Ro 2:29 *kutahiririwa* moyo kupitia roho
1Ko 7:19 *Kutahiririwa* hakuna maana, wala
TOKENI, Isa 52:11 *tokeni* humo, msiguse kitu kichafu!
Ufu 18:4 *Tokeni* kwake, watu wangu
TOLEO, Lu 7:37 *toleo* la nafaka
TOLEO LA KINYWAJI, Flp 2:17 kama *toleo la kinywaji*
TONGOZA, Met 7:21 *Anamtongoza* kwa maneno laini
TOSHA, 1Pe 4:3 wakati uliopitia *ulitwatosha* kufanya
TOWASHI, Mdo 8:27 *towashi* Mwehiotopia
TUBU, Lu 15:7 shangwe mtenda dhambi *anapotubu*
Mdo 3:19 *tubuni* na mgeuke ili
Mdo 17:30 kila mahali wanapaswa *kutubu*
Ufu 16:11 wakamkufuru Mungu, nao *hawakutubu*
TUKANA, 1Sa 17:26 hata *avitukane* vikosi vya Mungu
Ayu 2:5 kwa hakika *atakutukana*
Ayu 2:9 *Mtukane* Mungu, ufe!
1Pe 2:23 *Alipokutukana*, hakujibu kwa *kutukana*
TULIA, Ayu 37:14 *Tulia* na utafakari kazi za Mungu
TUMA, Isa 6:8 Mimi hapal *Nitume* mimi!
TUMAINI, Zb 9:10 wanaolijua jina lako *watakutumaini*
Zb 56:11 Katika Mungu ninaweka *tumaini*
Zb 62:8 *Mtumainini* nyakati zote
Zb 84:12 Mwenye furaha ni mtu *anayekutumaini*
Zb 146:3 *Msiwatumaini* waku
Zb 146:5 Mwenye furaha ni *anayemtumaini* Yehova
Met 3:26 *Anayemtumaini* moyo wake ni mpumbavu
Yer 17:5 Amelaaniwa *anayemtumaini* wanadamu
Ro 8:24 *tumaini* linaloonekana si *tumaini*
Ro 12:12 Shangilieni katika *tumaini*
Ro 15:4 kupitia uvumilivu witu tuwe na *tumaini*
Efe 1:18 mjue *tumaini* alilowaitia
Efe 2:12 hamkuwa na *tumaini* bila Mungu
Ebr 6:19 *tumaini* kama nanga ya nafsi
TUMBO, Flp 3:19 mungu wao ni *tumbo* lao
TUMIA, Iko 7:31 wale *wanaoutumia* ulimwengu
TUMIA VIBAYA, Lu 15:13 *akatumia vibaya* mali yake
TUMIKIA, Yos 24:15 chagueni yote *mtakayemtumikia*
1Nya 28:9 *kumtumikia* kwa moyo kamili
Zb 100:2 *Mtumikieni* Yehova kwa kushangilia
Gal 5:13 *Mtumikiane* kupitia upendo
TUNDA, Gal 5:22 *tunda* la roho ni upendo, shangwe
TUNDIKA, Angalia MTI.
TUNGA, Zb 94:20 *kinapotunga* matatizo kwa sheria?
TUNZA, Yoh 17:12 nilikuwa *nikiwatunza*
1Ko 12:25 bali viungo vyake *vitunzane*
Efe 5:29 huulisha na *kuuntunza*
TUZO, 1Ko 9:24 lakini ni mmoja tu *anayepokea tuzo*
Kol 2:18 Msimruhuse yeyote awanyang'anye *tuzo*
TWIKA, Lu 11:46 *mnaawatika* watu mizigo mizito

U

UA, Hes 35:6 *anayemuua* mwenzake akimbilie humo
Yoh 16:2 kila mtu *atakayewaua* atafikiri
UADILIFU, Zb 45:7 Ulipenda *uadilifu* na kukuchua uovu
Isa 26:9 Wakaaji wa nchi hujifunza *uadilifu*

Isa 32:1 Mfalme atatawala kwa *uadilifu*
 Isa 60:17 *uadilifu* kuwa watu wanaogawa kazi
 Sef 2:3 Uatufeni *uadilifu*, utafuteni upole
 2Pe 3:13 humo *uadilifu* utakaa
UADUI, Mwa 3:15 nitaweka *uadui* kati yako na
UAGUZI, Hes 23:23 hakuna *uaguzi* dhidi ya Israeli
 Kum 18:10 asipatikane yeyote anayefanya *uaguzi*
UAMINIFU, Hab 2:4 mwaadilifu ataishi kwa *uaminifu* wake
 Tit 2:10 wawe *waaminifu* kabisa
UASHERATI, Mt 15:19 moyoni hutoka *uasherati*
 Mdo 15:20 wajepushe na *uasherati* na damu
 Iko 5:9 mwache kushirikiana na *waasherati*
 1Ko 6:9 *Waasherati* hawataurithi Ufalme
 1Ko 6:18 Ukimbieni *uasherati*!
 1Ko 10:8 Wala tusifanye *uasherati*
 Gal 5:19 *uasherati*, uchafu, mwenendo mpotovu
 Efe 5:3 *Uasherati* usitajwe kati yenu
 1Th 4:3 mjepushe na *uasherati*
UASI, 1Sa 15:23 *uasi* ni sawa na dhambi ya *uaguzi*
UASI IMANI, 2Th 2:3 kabla *uasi imani* hauajitokea kwanza
UASI SHERIA, Mt 7:23 Ondokeni mnaotenda *uasi sheria*!
 Mt 24:12 sababu ya kuongezeka kwa *uasi sheria*
 2Th 2:3 mtu wa *uasi sheria* kufunuliwa
 2Th 2:7 fumbo la *uasi sheria* huu tayari
UBAGUZI, Mdo 10:34 Mungu hana *ubaguzi*
UBASHIRI, Kum 18:10 anayetafuta ishara za *ubashiri*
UBATILI, Mhu 1:2 *Ubatili* mkubwa kupita wote!
 Isa 41:29 Sanamu zao ni upepo na *ubatali*
 Efe 4:17 katika *ubatali* wa akili zao
UBATIZO, Ro 6:4 tulizikwa kupitia *ubatizo* katika kifo
 1Pe 3:21 *Ubatizo*, unawaokoa ninyi sasa
UBAVU, Mwa 2:22 akaufanya *ubavu* uwe mwanamke
UCHAFU, Ro 1:24 Mungu aliwaacha katika *uchafu*
 Kol 3:5 kuhusiana na *uasherati*, *uchafu*
UCHAWI, Kum 18:10 Asipatikane anayefanya *uchawi*
 Mdo 19:19 waliofanya *uchawi* wateketeza vitabu
UCHONGEZI, Law 19:16 Usizunguue kieneza *uchongezi*
UCHU, Ro 1:27 wanaume kwakiana tamaa kati za *uchu*
UCHUNGU, Kut 2:24 akasikia kilio chao cha *uchungu*
 Zb 78:40 kumtia *uchungu* jiangwani!
 Met 14:10 Moyo hujua *uchungu* wake
 Eze 9:4 wanaolia kwa *uchungu* na mamuvu makali
 Mt 26:75 akaenda nje akalia kwa *uchungu*
 Kol 3:19 msiwakasirikie kwa *uchungu*
UCHUNGUZI, Kum 13:14 kufanya *uchunguzi* kamili na
UDANGANYIFU, Efe 4:25 mmeacha *udanganyifu*
UDHAIFU, Ro 14:1 Mkaribisheni mtu aliye na *udhaifu*
 Ro 15:1 kubeba *udhaifu* wa wasio na nguvu
UDONGO, Isa 45:9 *udongo* kumuuliza Mfinyanzi
 Isa 64:8 Sisi ni *udongo*, nawe ni Mfinyanzi wetu
 Da 2:42 chuma na *udongo*
 Mt 13:23 iliyoandwa kwenye *udongo* mzuri
UELEWAJI, 1Fa 3:11 uliomba *uelewaji*
 Met 3:5 usitenge *uelewaji* wako mwenyewe
 Met 4:7 Pamoja na vyote, jipatie *uelewaji*
 Da 11:33 watawasaidia wengi kupata *uelewaji*
 1Ko 14:20 muwe watu wazima katika *uelewaji*
UENI, Kol 3:5 *viueni* viungu ywa mwili yenu
UFAHAMU, 1Fa 8:47 warudiwe na *ufahamu* na kukurudia
 Zb 119:9 Nina *ufahamu* kuliko walimu wangu
 Mt 19:11 *Ufahamu* wa mtu hutuliza hasira yake
 Da 12:3 walio na *ufahamu* watang'aa kama anga
UFALME, Kut 19:6 Mtaukuwa *ufalme* wa makuhani
 Da 2:44 Mungu wa mbinguni atausimamisha *ufalme*
 Da 7:14 akapewa utawala, heshima, na *ufalme*
 Da 7:18 watakatifu watapokea ule *ufalme*
 Mt 6:10 *Ufalme* wako na uje. Mapezi yako
 Mt 6:33 endeeleni kuatafuta kwanza *Ufalme*
 Mt 21:43 *Ufalme* kupewa taifa linalozaa matunda
 Mt 24:14 habari njema ya *Ufalme* itahubiriwa
 Mt 25:34 Njoni, urithini *Ufalme* uliotayarishwa
 Lu 12:32 amekubali kuwapa *Ufalme*
 Lu 22:29 ninafanya agano nanyi, la *ufalme*
 Yoh 18:36 *Ufalme* wangu si sehemu ya ulimwengu
 Mdo 1:6 je, unaurudisha *ufalme* kwa Israeli
 1Ko 15:24 atakapoukabidhi *Ufalme* kwa Mungu
 Gal 5:21 hawataurithi *Ufalme* wa Mungu

Kol 1:13 kutuingiza katika *ufalme* wa Mwana wake
 Ufu 1:6 alitufanya tuwe *ufalme*, makuhani kwa
 Ufu 11:15 *Ufalme* wa ulimwengu umekuwa *Ufalme*
UFASAHA, Kut 4:10 sijawahi kusema kwa *ufasaha*
UFASADI, Da 6:4 hakuwa mzembe wala *mfisadi*
UFUFUO, Mt 22:23 Masadukayo husema hakuna *ufufuo*
 Mt 22:30 katika *ufufuo*, wanaume hawaoi
 Yoh 5:29 kwenye *ufufuo* wa uzima
 Yoh 6:39 *niwafufue* katika siku ya mwisho
 Yoh 11:24 atafufuka katika *ufufuo* siku ya mwisho
 Yoh 11:25 Mimi ndiye *ufufuo* na uzima
 Mdo 2:24 Mungu alimfufua
 Mdo 24:15 *ufufuo* wa waadilifu na wasio waadilifu
 1Ko 15:13 ikiwa hakuna *ufufuo*, Kristo hakufufuliwa
UFUNGUO, Lu 11:52 mliuondoa *ufunguo* wa ujuzi
UGOMVI, Met 6:19 anayepanda *ugomvi* miongoni
 Met 15:18 asiyekasirika upesi hutuliza *ugomvi*
 Met 17:14 Kabla *ugomvi* haujalipuka, ondoka
 Mdo 15:39 wakagombana kwa ukali
UGONJWA, Mt 9:35 kuponya kila aina ya *ugonji*
UGUMU, Mt 13:15 miyo ya watu imekuwa *migumu*
UHAJ, Zb 36:9 Wewe ndiye chanzo cha *uhaji*
 Lu 9:24 anayetaka kuokoa *uhaji* atapoteza
 Mdo 20:24 sioni *uhaji* wangu kuwa muhimu
UHAKIKA, Mt 3:26 Yehova chanzo cha *uhakika* wako
 Mhu 7:14 *uhakika* kuhusu jambo lolote litakalowapata
 Ro 4:21 akiwa na *uhakika* kamili kwamba Mungu
 2Th 3:4 tuna *uhakika* katika Bwana kwahusu ninyi
UHAKIKISHO, Mdo 17:31 *uhakikisho* kwa kumfua
UHARAKA, 2Ti 4:2 fanya hivyo kwa *uharaka* nyakati
UHARIBIFU, 2Th 1:9 adhabu ya *uharibifu* wa milele
UHASAMA, Efe 4:31 chuki yenye *uhasama*, hasira
UHODARI, 2Ko 5:6 tuna *uhodari* mwingi
 Flp 1:14 *uhodari* mwingi wa kulisema neno la Mungu
UHURU, Ro 8:21 *uhuru* wenye utukufu wa watoto
 2Ko 3:17 palipo na roho ya Yehova, pana *uhuru*
 1Pe 2:16 msitumie *uhuru* wenu kama kifuniko
 2Pe 2:19 Wanawaadhi *uhuru*
UJANA, 1Ti 4:12 watu yeyote asidharu *ujana* wako
UJASIRI, Mt 28:1 waadilifu wana *ujasiri* kama simba
 Mdo 4:31 wakitangaza neno la Mungu kwa *ujasiri*
 Efe 6:20 niweze kuzungumza kuhusu kwa *ujasiri*
 1Th 2:2 tulijipa *ujasiri* kupitia Mungu wetu
UJINGA, Mt 19:3 *Ujinga* wa mtu hupotosha njia yake
 Mt 22:15 *Ujinga* katika moyo wa mvulana
UJITOAJI KAMILI
 Wim 8:6 *ujitooji kamili* haukubali kushindwa
UJITOAJI-KIMUNGU, 1Ti 4:7 lengo la *ujitooji-kimungu*
 1Ti 4:8 *ujitooji-kimungu* una faida
 1Ti 6:6 kuna faida kubwa ya *ujitooji-kimungu*
 2Ti 3:12 wanaoishi kwa *ujitooji-kimungu* wataeswa
UJUZI, Met 1:7 Kumwogopa Yehova, mwanzo wa *ujuzi*
 Met 2:10 *ujuzi* kupendelea nafsi yako
 Met 24:5 kwa *ujuzi* mtu huzidisha nguvu zake
 Isa 5:13 enda uhamishoni kwa kukosa *ujuzi*
 Isa 11:9 dunia itajaa *ujuzi* kumhusu Yehova
 Da 12:4 *ujuzi* wa kweli utakuwa mwingi
 Ho 4:6 Kwa sababu mmekataa *ujuzi*
 Mal 2:7 midomo ya kuhani kulinga *ujuzi*
 Lu 11:52 mliuondoa *ufunguo* wa *ujuzi*
 1Ko 8:1 *Ujuzi* huleta majiwu, upendo hujenga
 1Ti 1:13 nilitenda bila *ujuzi* na sikwa na imani
UJUZI SAHIMI, Ro 10:2 si kulingana na *ujuzi sahihi*
 Kol 3:10 utu kuwa mpya kupitia *ujuzi sahihi*
 1Ti 2:4 mapezi yake ni watu wapate *ujuzi sahihi*
UKAME, Yer 17:8 mahangaiko mwaka wa *ukame*
UKAMILI, 1Th 4:1 kufanya hivyo kwa *ukamili* zaidi
 1Th 4:10 endeeleni kufanya kwa *ukamili*
UKANDAMIZAJI, Zb 72:14 *ukandamizaji* na ukatili
 Mhu 7:7 *ukandamizaji*, mwenye hekima awe wazimu
UKARIMU, Kum 15:8 kumfumbulia mkono kwa *ukarimu*
 Mt 11:24 anayetoa kwa *ukarimu* hupata vitu vingi
 Yak 1:5 Mungu, huwapa wote kwa *ukarimu*
UKATILI, Mwa 6:11 dunia ilikuwa imejaa *ukatili*
 Zb 11:5 humchukia mtu anayependa *ukatili*
 Zb 72:14 kutoka katika *ukandamizaji* na *ukatili*
UKINGO, Law 23:22 msivune *kingo* wa mashamba yenu
UKOMA, Law 13:45 mwenye *ukoma*, si safi, si safi

Hes 12:10 Miriamu alipigwa kwa ukoma
 Lu 5:12 mwanamume aliyepaja ukoma!
UKOMAVU, Ebr 6:1 tusonge mbele kuelekea ukomavu
UKOMBOZI, Est 4:14 ukombozi kutoka chanzo kingine
 Lu 21:28 ukombozi wenu unakaribia
UKOO, Mdo 10:24 Kornelio amekusanya watu wa ukoo
UKUHANI, 1Pe 2:9 *ukuhani* wa kifalme, taifa takatifu
UKUNGU, Yak 4:14 ninyi ni *ukungu* unaoтока kwa muda
UKUTA, Yos 6:5 *ukuta* wa jiji utauangka chini
 Eze 38:11 wanaoishi bila kulindwa na *ukuta*, makomeo
 Da 5:5 kuandika kwenye *ukuta* wa mfalme
 Yoe 2:7 Wanapanda *ukuta* kama wanajeshi
UKWELI, Zb 15:2 kusema *ukweli* moyoni mwake
 Efe 4:25 semeni *ukweli* kila mmoja na mwenzake
ULIMI, Zb 34:13 ulinde *ulimi* wako usiseme mabaya
 Met 18:21 Kifo na uhai katika nguvu za *ulimi*
 Isa 35:6 *ulimi* wa bubu utapiga vigelegele
 Isa 50:4 amenipa *ulimi* wa waliofundishwa
 Yak 1:26 haudhibiti kabisa *ulimi* wake
 Yak 3:8 hakuna anayeweza kufuga *ulimi*
ULIMWENGU, Lu 9:25 akiupata *ulimwengu* wote lakini
 Yoh 15:19 si sehemu ya *ulimwengu*, unawachukua
 Yoh 17:16 Wao si sehemu ya *ulimwengu*
 1Yo 2:15 Msiupende *ulimwengu* wa
 1Yo 2:17 *ulimwengu* unapitilia mbali
ULINZI, Mhu 7:12 hekima ni *ulinsi* kama pesa
UMA, Gal 5:15 mnaendelea *kuumana* na kururuana
UMALIZIO, Mhu 12:13 Huu ndio *umalizio*
 Mt 28:20 nipo pamoja nanyi pamoja *umalizio* wa mfumo
UMANDE, Kum 32:2 Maneno yatadondoka kama *umande*
 Zb 110:3 vijana matone ya *umande*
UMASKINI, Met 30:8 Usinipe *umaskini* wala utajiri
 2Ko 8:2 *umaskini* wau ulifanya ukirumu uwe mwangi
UMATI, Kut 23:2 Usiufuate *umati*
UMATI MKUBWA, Ufu 7:9 *umati mkubwa*, kuuhesabu
UMBA, Mwa 1:1 Hapo mwanzo Mungu *alumba*
 Zb 104:30 Ukuituma roho yako, *wanaumba*
 Isa 45:18 Ambaye *hakuiumba* tu bila sababu
 Kol 1:16 kupitia kwake vitu vingine vyote *viliumbwa*
 Ufu 4:11 kwa sababu *ulumba* vitu vyote
UMIA, 1Ko 12:26 ukio kimoja *kikiumba*, vingine
UMILELE, Mhu 3:11 ameweka *umilele* katika moyo wao
UMOJA, Zb 133:1 Ndugu kukaa pamoja kwa *umoja*
 Efe 4:3 mkijitahidi kudumisha roho ya *umoja*
 Efe 4:13 mpaka sote tuwe na *umoja* katika imani
UNABII, Yoe 2:28 wana na mabinti watatoka *unabii*
 2Pe 1:20 *unabii* wa Andiko kutokana na fasiri
 2Pe 1:21 *unabii* haukuletwa na mwanadamu
UNAFIKI, Ro 12:9 Upendo wenu na uwe bila *unafiki*
UNAJISI, 2Ko 7:1 tujisafishe kila *unajisi*
UNAOCHUKIZA, Hes 21:5 mkate huu *unaochukiza*
UNASTAHILI, Ufu 4:11 *Unastahili*, Ee Yehova
UNGAMA, Zb 32:5 Mwishowe *nikaungama* dhambi yangu
 Met 28:13 *anayeaungama* ataonyesha rehema
 Yak 5:16 *ungameni* dhambi zenu
 1Yo 1:9 *Tukiungama* dhambi zetu, atatusamehe
UNGANISHA, Mt 19:6 kile Mungu *ameunganisha*
UNGANISHWA, Efe 4:16 mwili wote *unanganishwa*
 Flp 2:2 mkiwa *mmeunganishwa* kabisa
UNYAKUZI, Flp 2:6 hakufikiria kufanya *unyakuzi*
UNYASI, Mt 7:3 *unyasi* katika jicho la ndugu yako
UNYENYEKEVU, Met 15:33 kabla utukufu, *unyenyekevu*
UNYOOFU, Ayu 1:8 Ayubu ni *mnyoofu* na mtimilifu
 2Ko 8:21 tunashughulikia mnyoofu wote kwa *unyoofu*
 Ebr 13:18 kujijendesha kwa *unyoofu* katika mambo yote
UOYU, 1Th 5:22 Epukeni kila aina ya *uoyu*
UPANGA, 1Sa 17:47 Yehova haokoi kwa *upanga*
 Mt 26:52 wanaochukua *upanga* wataangamia
 Efe 6:17 *upanga* wa roho, neno la Mungu
 Ebr 4:12 neno la Mungu, makali kuliko *upanga*
UPARA, Law 13:40 Ikiwa mwanamume atapata *upara*
 Law 21:5 Hawapaswi kunyoka *upara*
 2Fa 2:23 Panda, weve mwenye *upara!*
UPATANISHO, Ro 3:25 kuwa dhahabu ya *upatanisho*
 1Yo 2:2 Nayen dhahabu ya *upatanisho*
UPATANO, 1Ko 1:10 mseme kwa *upatano*
UPENDELEO, Yak 2:9 mkiendelea kuonyesha *upendeleo*
UPENDO, Wim 8:6 *upendo* una nguvu kama kifo
 Mt 24:12 hapuna wa wengi utapoa

Yoh 15:13 Hakuna aliye na *upendo* mkuu kuliko
 Ro 8:39 kututenga na *upendo* wa Mungu
 Ro 12:10 Katika *upendo* wa kindugu
 Ro 13:10 *upendo* ndio utimizwa wa sheria
 1Ko 8:1 Ujuzi huleta majiuvu, *upendo* hujenga
 1Ko 13:2 ikiwa sina *upendo*, mimi si kitu
 1Ko 13:13 *upendo* haushindwi kamwe
 1Ko 13:13 lililo kubwa zaidi kati ya hayo ni *upendo*
 1Ko 16:14 fanyeni mambo yote kwa *upendo*
 2Ko 2:8 mthibitishieni *upendo* wenu
 Kol 3:14 *upendo* ni kifungo kikamilifu
 1Pe 4:8 *upendo* hufunika dhambi nyingi
 1Yo 4:8 Mungu ni *upendo*
 Yud 21 kujitunza katika *upendo* wa Mungu
 Ufu 2:4 umeacha *upendo* uliokuwa nao
UPENDO MSHIKAMANIFU
 Kut 34:6 upendo mwingi *mshikamanifu*
 Zb 13:5 ninautumaini *upendo* wako *mshikamanifu*
 Zb 136:1-26 *Upendo* wake *mshikamanifu* unadumu
 Ho 6:6 ninapendezwa na *upendo* *mshikamanifu*
UPENDO MWORORO, Kol 3:12 jivikeni *upendo* *mwororo*
 Yak 5:11 Yehova ni mwenye *upendo* *mwororo*
UPEO, 1Ko 7:36 amepita *upeo* wa ujana
UPEO, Mhu 11:4 Anayeaungalia *upeo* hatapanda
 Mt 7:25 *upeo* ukavuma na kipaupiga nyumba hiyo
 Efe 4:14 kupeperushwa na kulipewa wa fundishi
UPINDE WA MVUA, Mwa 9:13 *upinde* wangu wa mvua
UPINDO, Hes 15:39 kutengeza *upindo* huo
UPINZANI, 1Th 2:2 tulijipa ujasi licha ya *upinzani*
UPOFU, Mwa 19:11 wakawapiga kwa *upofu* wanaume
UPOLE, 1Ko 4:13 tunapochongewa, tunajibu kwa *upole*
 1Th 7:2 *upole*, kama mama anayenyonyesha
 1Pe 3:4 roho ya utulivu na ya *upole*
UPOTOVU, Met 1:32 *upotovu* wa wajinga utawaua
UPUMBAVU, 1Ko 3:19 ya ulimwengu, *upumbavu*
UPUZI, Lu 24:11 waliyoona kama maneno ya *upuuzi*
URAFIKI, Zb 25:14 *Urafiki* wa karibu na Yehova ni wa
 Met 3:32 ana *urafiki* wa karibu na wanyoofu
 Yak 4:4 *urafiki* na ulimwengu ni uadui na Mungu
URAI, Flp 3:20 *uraila* wete uko mbungini
UREMBO, Met 6:25 Usiutumaini *urembo* wake moyoni
 Mt 31:30 huenda *urembo* ukatoweka upesi
 Eze 18:21 moyo wa majiuvu kwa sababu ya *urembo*
URIMU NA THUMIMU, Kut 28:30 *Urimu* na *Thumimu*
URITHI, Hes 18:20 Mimi ni fungu lako na *urithi* wako
 Zb 127:3 Watoto ni *urithi* kutoka kwa Yehova
 Efe 1:18 utajiri wenyte utukufu *urithi* wa watakatifu
 Ebr 10:34 mna *urithi* bora na wenyte kudumu
 1Pe 1:4 *urithi* usioharibika na usio na unajisi
USADIKISHO, Ro 8:38 *nimesadiki* kwamba wala kifo
 Ro 15:14 *nimesadiki* kuwahusu, ndugu zangu
 Kol 4:12 *usadikisho* katika mapenzi ya Mungu
 1Th 1:5 kwa roho takatifu na kwa *usadikisho* thabiti
USALAMA, 1Fa 4:25 Israeli walishi kwa *usalama*
 Met 3:23 Ndipo utakapoteamba kwa *usalama*
 Isa 32:17 mazao ya uadilifu, *usalama* wa kudumu
 Ho 2:18 nitawafanya waishi kwa *usalama*
 Flp 3:1 nawaandikia kwa ajili ya *usalama* wenu
USAWAZIKO, Flp 4:5 *Usawaziko* wenu na ujulikane
USAWAZISHO, 2Ko 8:14 ili kuwe na *usawazisho*
USHAHIDI, Mt 24:14 Ufalme utahubiriwa kwa *ushahidi*
 Yoh 7:7 ulimwengu unanichukia, ninatoka *ushahidi*
 Yoh 18:37 ili nitoe *ushahidi* kuhusu kweli
 Mdo 10:42 alitumuru tubhiri na kutoa *ushahidi* kamili
 Mdo 28:23 kutoa *ushahidi* kamili kuhusu Ufalme
USHIKAMANIFU, Mik 6:8 uthamini sana *ushikamanifu*
USHINDI, 2Ko 2:14 maandamano ya *ushindi*
USHIRIKA, 1Pe 2:17 upendeni *ushirika* mzima
USHIRIKIANO, Ro 8:28 hufanya kazi zote *zishirikiane*
 Efe 4:16 *kushirikiana* kila ujango
USHUPAVU, 2Pe 2:10 Wana ujaoji na *ushupavu*
USIKU, Zb 19:2 *usiku* baada ya *usiku* zinafutua ujuzi
 Ro 13:12 *Usiku* umesonga; mchana umekaribia
USIMAMIZI, Efe 1:10 kwa ajili ya *usimamizi*
USINGIZI, Ro 13:11 saa ya kuamka kutoka *usingizini*
USIU, Kut 20:13 *Usiue*
USIWANYIME, Met 3:27 *Usiwanyime* mema wale
USTADI, Kut 35:35 Amewajaza *ustadi* wa kufanya kazi
 2Ti 4:2 kwa sabira na *ustadi* wa kufundisha

UTAJIRI, Met 11:28 Anayeutumaini utajiri ataanguka
Met 30:8 Usinipe umaskini wala utajiri
Eze 28:5 moyo ukawa na majivuno kwa utajiri
Mt 6:24 Hamwezi kutumikia Mungu na utajiri
Mt 13:22 nguvu za udanganyifu za utajiri
UTAKASO, Ebr 12:14 Fuatilieni utakaso
UTAMBI, Isa 42:3 hatazima utambi unaofia
UTAMBUZI, Mt 24:15 msomaji na atumie utambuzi
UTARATIBU, 1Nya 15:13 hatukutafuta utaratibu unaofaa
Lu 1:3 kukuandikia kwa utaratibu mzuri
Gal 5:25 kutembea kwa utaratibu kwa roho
1Th 5:14 waonyeni wale wasiofuata utaratibu
2Th 3:6 mjiepushie na ndugu asiyefuata utaratibu
1Ti 3:2 Mwangalizi anapaswa kuwa mwenye utaratibu
UTAWALA, Isa 9:7 Kwa wingi wa utawala wake
Da 4:34 utawala wake ni utawala wa milele
UTAYARI, Zb 51:12 Chochea utayari wa kukuti
2Ko 8:12 ikiwa utayari upo kwanza
UTELEZI, Zb 73:18 weka kwenye ardi ya utelezi
UTENDAJI, 1Pe 1:13 kazenzi akili zenu kwa ajili ya utendaji
UTHAMINI, Zb 27:4 kutazama kwa uthamini hekalu
UTIMILIFU, 1Nya 29:17 unapendezwa na utimilifu
Ayu 27:5 Mpaka nife, sitaukana utimilifu wangu
Zb 25:21 Utimilifu na unyofu na viniliende
Zb 26:11 nitatembea katika utimilifu wangu
Zb 101:2 Nitatembea kwa utimilifu ndani ya nyumba
UTOTO, 2Ti 3:15 tangu utoto umeyajua maandishi
UTU, Efe 4:24 mnapaswa kuvaa utu mpya
Kol 3:9 Uvueni utu wa zamani
UTUKUFU, Yoh 12:43 utukufu wa wanadamu
Ro 3:23 kupungukiwa na utukufu wa Mungu,
Ro 8:18 si kitu yakilinganisha na utukufu
1Ko 10:31 fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu
Ufu 4:11 Unastahili, Yehova kupokea utukufu
UTULIVU, Met 14:30 Moyo mtulivu huupa mwili uzima
Met 17:27 mtu mwenye utambuzi atabaki mtulivu
1Th 4:11 lengo la kuishi kwa utulivu
1Pe 3:4 roho ya utulivu na ya upole
UTUMISHI MTAKATIFU, Ro 12:1 utumishi mtaakatifu na
UTUSITUSI, Sef 1:15 Siku ya giza na utusitusi
UUMBARI, Ro 1:20 zinaonekana tangu kuumbwa kwa
Ro 8:20 uumbaji ulitishwa chini ya ubatili
2Ko 5:17 muungano na Kristo, yeye ni kiumba kipyaa
Kol 1:23 katika uumbaji wote chini ya mbingu
Ufu 3:14 mwanzo wa uumbaji wa Mungu
UVUMILIVU, Lu 8:15 kuzaa matunda kwa uvumilivu
Lu 21:19 Mkivumilia, mtaouko uhai wenu
Ro 5:3 dhiki hutokeza uvumilivu
Yak 1:4 acheni uvumilivu ukamilishe kazi yake
Yak 5:11 Mmesikia kuhusu uvumilivu wa Ayubu
UWEZO, Zb 40:17 Lakini sina uwezo, nami ni maskini
Met 3:27 Usiwanjime mema, ikiwa una uwezo
Mt 25:15 talanta kulingana na uwezo wao
UWEZO WA KUFIKIRI, Met 1:4 kumpa uwezo wa kufikiri
UWONGO, Zb 34:13 Midomo yako isiseme uwongo
Mt 26:59 Sanhedrini ikitafulu ushahidi wa uwongo
Gal 2:4 ndugu wa uwongo walioingizwa kimyakimya
Kol 3:9 Msiambiane uwongo
2Th 2:11 hivyo waamini uwongo
2Ti 2:2 Mungu, asiyeweza kusema uwongo
2Pe 2:3 wakisema maneno ya uwongo
UZAO, Mwa 3:15 uadui kati ya uzao wako na mwanamke
Mwa 22:17 nitaufanya uzao wako uwe mwingi
Isa 65:23 uzao wa watu waliobarikwa na Yehova
Gal 3:16 na kwa uzao wake, ambaye ni Kristo
Gal 3:29 kwa kweli ni uzao wa Abrahamu
UZEE, Zb 71:9 Usinitupe wakati wa uzee
UZEEINI, Zb 92:14 wakati wa uzeeni watanawiri
UZEMBE, Yer 48:10 anayefanya kazi kwa uzembe!
UZIA, 2Nya 26:21 Mfalme Uzia alikuwa na ukoma
UZIMA, Kum 30:19 nimeweka uzima na kifo mbele yenu
Yoh 5:26 Baba aliyvo na uzima ndani yake
Yoh 11:25 Mimi ndiye ufufu na uzima
UZIMA WA MILELE, Da 12:2 watapata uzima wa milele
Lu 18:30 mara nyingi wakati huu, na uzima wa milele
Yoh 3:16 asiangamizwe bali awe na uzima wa milele
Yoh 17:3 Uzima wa milele ndio huu
Mdo 13:48 mweleke unaofaa uzima wa milele

Ro 6:23 Mungu hutoa uzima wa milele
1Ti 6:12 ushike imara uzima wa milele
UZINZI, Kut 20:14 Usifanye uzinzi
Mt 5:28 tayari amefanya uzinzi moyoni
Mt 19:9 na kumwoa mwingine, anafanya uzinzi
UZITO, Ebr 12:1 tuondoe kila uzito
UZOEUFU, Zb 19:7 asiye na uzoeufu awe na hekima

V

VAA, Met 7:10 Akiwa ameava kama kahaba
VEMA, Mt 25:21 Vema, mtumia mwema na mwaminifu!
VIFAA, 2Ti 3:17 vifaa kamili kwa ajili ya kila kazi njema
Ebr 13:21 awape vifaa vyote vyema ili
VIJANA, Zb 110:3 vijana kama matone ya umande
Met 20:29 Utukufu wa vijana ni nguvu zao
VIKAPU, Mt 14:20 vilivyobaki, wakajaza vikapu 12
VIKUMBUSHO, Zb 119:24 Ninavipenda vikumbusho
VIKWAZO, 1Ko 10:32 Epukeni kuwa vikwazo
VILEMA, Mt 15:31 vilema wakiponywa
VINYONGE, 1Ko 1:28 Mungu alivichagua vitu vinyonge
VIOO, 2Ko 3:18 toa kama vioo mrudisho wa utukufu wa
VIPYA, Ufu 21:5 Ninafanya vitu vyote kuwa vipya
VITA, 1Sa 17:47 vita ni vya Yehova
Zb 46:9 Anakomesha vita
Isa 2:4 Wala hawatajifunga vita tena
Ho 2:18 Nitaondoa upanga na vita nchini
1Ko 14:8 ni nani atajitayarisha kwa vita?
Ufu 12:7 vita vikatokea ghafla mbinguni: Mikaeli
Ufu 16:14 vita vya siku kuwa ya Mungu
VITABU, Mhu 12:12 Hakuna mwisho wa kutunga vitabu
Mdo 19:19 wakavitekeza vitabu vyao mbele ya
Ufu 20:12 vitabu vya kukunja
VITISHO, Zb 91:5 Hutaogopa vitisho vya usiku
1Pe 2:23 Alipoteseka, hakutoa vitisho
VITI VYA UFALME, Da 7:9 viti vya ufalme vikawekwa
VITU VINGI, Lu 12:15 mtu anapokuwa na vitu vingi
VITU VISIVYOONEKANA, 2Ko 4:18 vitu visivyoonekana
VUA, Lu 5:10 Kuanzia sasa utakuwa ukivauwa watu
VUGUVUGU, Ufu 3:16 kwa sababu wewe ni vuguvugu
VUMILIA, 2Fa 10:16 sivumilii ushindani wowote
Hab 1:13 huwezi kuvumilia uovu
Mt 24:13 atakayevumilia mpaka mwisho ndiye
Ro 9:22 Mungu alivumilia vyoombu vya ghadhabu
Ro 12:12 Vumilieni chini ya dhiki
1Ko 4:12 tunapoteswa, tunavumilia kwa subira
1Pe 2:20 mnavumilia mateso kwa sababu ya
VUMILIANA, Efe 4:2 mkivumiliana kwa upendo
VUNA, Mhu 11:4 anayetazama mawingu hatavuna
Ho 8:7 wanapanda upepo, watavuna kimbunga
2Ko 9:6 anayepanda kwa uhaba atavuna kwa uhaba
Gal 6:7 analopanda mtu, ndilo atakalovuna
Gal 6:9 tutavuna ikiwa hatutachoka kabisa
VUNJIKIA, Zb 51:17 Dhabihu, roho iliyovunjika
Met 29:1 shingo ngumu itavunjika kwa ghafla
1Ti 1:19 imani yao ikavunjika
VUNJIKI MOYO, 2Nya 15:7 iweni imara msivunjike moyo
Zb 34:18 karibu na waliovunjika moyo
Met 24:10 Ukivunjika moyo siku ya taabu
Kol 3:21 watoto wenu wasivunjike moyo
VUTA, Yoh 6:44 isipokuwa Baba aliyenituma amvute
VYAKULA BORA, Da 1:5 wapewe vyakula bora
VYUMBA, Isa 26:20 ingieni, vyumba vyenu vya ndani

W

WAADILIFU, 1Pe 3:12 Yehova anawatazama waadilifu
WAANGALIFU, Mt 10:16 iweni wangaalifu kama nyoka
WAANGALIZI, Isa 60:17 amani kuwa waangalizi
Mdo 20:28 roho takatifu imewaweka muwe waangalizi
1Pe 5:2 mkiwa waangalizi, kwa hari
WAASI, Hes 20:10 Sikilizeni sasa, enyi waasi
Met 24:21 usishirikiane na waasi
WAASI SHERIA, Lu 22:37 alihesabiwa na waasi sheria
WABASHIRI, Law 19:31 msitafute ushauri kwa wabashiri
WACHUNGAJI, Eze 34:2 wachungaji wanaojilisha
Efe 4:11 wengine wachungaji na walimu
WACHUZZI, 2Ko 2:17 sisi si wachuzi wa neno la Mungu
WADHIHAKI, Zb 3:3 siku za mwisho wadhikaki watakuja

WAFALME, Met 22:29 Husimama mbele ya *wafalme*
 Lu 21:12 Mtappekwa mbele ya *wafalme* na magavana
 Mdo 4:26 *Wafalme* wa dunia walijipanga
 Ufu 5:10 watakuwa *wafalme* juu ya dunia
 Ufu 18:3 *wafalme* wa dunia walifanya uasherati naye
WAFANYABIASHARA, Ufu 18:3 *wafanyabiashara*
WAFANYAKAZI, 1Ko 3:9 *wafanyakazi* wenzi wa Mungu
WAFARJI, Ayu 16:2 Ninyi ni *wafarji* wasumbufu!
WAGENI, Yoh 10:5 hawajui sauti ya *wageni*
WAGUMU, Mdo 19:9 wakawa *wagumu*, wakakataa
WAHUDUMU, 2Ko 3:6 ametustahilisha kuwa *wahudumu*
 2Ko 6:4 tunajipendeleza kuwa *wahudumu* wa Mungu
WAIGAJI, 1Ko 11:1 Iweni *waigaji* wangu, kama
 Efe 5:1 iweni *waigaji* wa Mungu, kama watoto
WAIMBAJI, 1Nya 15:16 akawaambia waweke *waimbaji*
WAJANE, Yak 1:27 kuwatunga mayatima na wajane
WAJIBIKA, 1Sa 22:22 *ninawajibika* kwa sababu ya kifo
WAJIBU, Mhu 12:13 wajibu wote wa mwanadamu
 1Yo 3:16 wajibu kutoa ahi wetu kwa ajili ya ndugu
WAJINGA, Met 22:3 wajinga kupata madhara
WAKA, Ro 12:11 *Wakeni* roho
WAKALIMANI, 1Ko 12:30 Je, wote ni *wakalimani*?
WAKARIMU, 1Ti 6:18 wawe *wakarimu*, tayari kushiriki
WAKATI, Mhu 3:1 *Wakati* wa kila shughuli
 Mhu 9:11 *wakati* na matukio yasiyotarajiwa
 Da 7:25 *wakati*, nyakati, na nusu *wakati*
 Yoh 7:8 *wakati* wangu haujafika kikamili
 1Ko 7:29 *wakati* uliobaki umezunguza
 Efe 5:16 mkiumia vizuri *wakati* wenu
WAKATILI, Zb 5:6 Yehova anawachukia *wakatili*
WAKATI UJAO, Zb 7:17 nikatambua *wakati* wao ujao
 Met 24:20 mwovu hana *wakati* ujao
WAKATI ULIOWEKWA, Hab 2:3 yatimbia *wakati uliowekwa*
WAKATI UNAOFAA, Lu 4:13 mpaka *wakati unaofaa*
WAKE, 1Fa 11:3 alikuwa na *wake* 700 na masuria 300
 Efe 5:22 *Wake* wajitishie kwa waume zao
 Efe 5:28 kuwependa *wake* kama mlii yoo
WAKILI MKUU, Mdo 3:15 milimua *Wakili Mkuu* wa uzima
 Ebr 12:2 *Wakili Mkuu* na Mkamilishaji wa imani yetu
WAKOMAVU, Ebr 5:4 *wakomavu*, wamezoza nguvu za
WAKRISTO, Mdo 11:26 waliitwa *Wakristo* kupitia
WAKUJU, Zb 45:16 Utawaweka kuwa *waku* duniani
 Isa 32:1 *waku* watawala kwa haki
WALALAMIKAJI, Yud 16 wanung'unikaji, *walalamikaji*
WALAWI, Kut 32:26 *Walawi* wote wakakusanyika
 Hes 3:12 *Walawi* watakuwa wangu
 2Nya 35:3 *Walawi*, walimu wa Waisraeli wote
WALEVI, 1Ko 6:10 *walevi* hawataurithi Ufalme
WALIMU, Zb 119:99 ufahamu kuliko *walimu* wangu
 Efe 4:11 wengine wawe *walimu*
WALIOBAKI, Ufu 12:17 akapigana na waliobaki
WALIOCHAGULIWA, Mt 24:22 sababu ya waliochaguliwa
 Mt 24:31 malaika watawakusanya waliochaguliwa
WALIOVUNJIKA MOYO, Zb 147:3 Huponya waliovunjika moyo
WAMEINGIA KISIRI, Yud 4 watu fulani wameingia kisiri
WANA, Mwa 6:2 wana wa Mungu wakachukua wake
 1Sa 8:3 *wanawe* hawakufuta njia zake
 Ayu 38:7 *wana* wa Mungu wakashangilia
 Isa 54:13 *wana* wako wote watafundishwa na Yehova
 Isa 66:8 Sayuni aliwazaa *wanawe*
 Ro 8:14 wanaoongozwa na roho ni *wana*
 Ro 8:15 roho ya kufanywa kuwa *wana*
WANAFALSIFA, Mdo 17:18 Waepikurea na wanafalsifa
WANAFUNZI, Mt 28:19 nendeni mkafanye wanafunzi
 Yoh 8:31 ninyi ni wanafunzi wangu
 Yoh 13:35 ninyi ni wanafunzi wangu—mkiwa na upendo
WANAJIMU, Mt 2:1 wanajimu walikuja Yerusalemu
WANAKONDOO, Isa 40:11 Atawakusanya wanakonoo
 Yoh 21:15 Lisha wanakonoo wangu
WANANCHI, 1Th 2:14 militesha na wananchi wenzenu
WANAORUDI NYUMA, Ebr 10:39 si watu wanaorudi nyuma
WANAUME, 1Ko 6:9 wanaofanya ngono na wanaume
 1Ko 16:13 endeleeni kuwa kama wanaume
WANAWAKE, Kum 31:12 Kusanya wanaume, wanawake
 Met 31:3 Usiwape wanawake nguvu zako
 Met 31:29 umewapita wanawake wengi
WANEFILI, Mwa 6:4 Wanefili walikuwa duniani siku hizi

WANUNG'UNIKAJI, 1Ko 10:10 tusiwe wanung'unikaji
 Yud 16 Watu hawa ni wanung'unikaji
WANYAMA, Law 26:6 nitawaondoa wanyama wote
 Met 12:10 Mwadilifu huwatunza wanyama
 Mhu 3:19 wanadamu na wanyama; mwisho uleule
 Eze 34:25 atawaondoa nchini wanyama hatari
 Da 7:3 wanyama wanoe wakubwa wakatoka baharini
 Ho 2:18 agano na wanyama wa mwituni
WANYENYEKEVU, Yak 4:6 wanyenyekevu, fadhili
WAOVU, Zb 37:9 Kwa maana waovu wataangamizwa
 Zb 37:10 watu waovu hawatakupelewa tena
 Met 15:8 Dhahibu ya waovu humchukiza Yehova
 Met 15:29 Yehova yuko mbali na waovu
 Isa 57:21 Hakuna amani kwa waovu
 Ro 12:17 Msimilpe yeyote uovu kwa uovu
WAPINGA-KRISTO, 1Yo 2:18 wapinga-Kristo wengi
WAPINZANI, Lu 21:15 hekima ambayo wapinzani
 1Ko 16:9 kuna wapinzani wengi
 Flo 1:28 bila kuogopesha wamne na wapinzani
WAPOLE, Zb 37:11 wapole watamiliki dunia
 Sef 2:3 Mtafuteni Yehova, wapole wa dunia
WAREKABU, Yer 35:5 weka divai mbele ya Warekabu
WARITHI, Ro 8:17 warithi wa Mungu, warithi na Kristo
 Gal 3:29 uzao wa Abrahamu, warithi wa ahadi
WASEJA, 1Ko 7:8 ninawaambia waseja na wajane
WASHAIRI, Mdo 17:28 washairi wenu wamesema
WASHAURI, Met 15:22 hufanikiwa kupitia washauri
WASHIKAMANIFU, 1Sa 2:9 Hulinda washikamanifu
 Zb 37:28 Yehova washikamanifu wake
WASIKIVU, Mdo 17:11 wasikivu kuliko wa Thesalonike
WASIMAMIZI, 1Ko 4:2 wasimamizi, wakiwa waaminifu
WASIOFAA KITU, Lu 17:10 watumwa wasiofaa kitu
WASIOGOTIA, 2Pe 1:8 msiwe wasiogotia, wasiozaa
WASIO WAADILIFU, Mdo 24:15 wasio waadilifu
 1Ko 6:9 wasio waadilifu hawataurithi Ufalme
WASIO WAAMINI, 1Ko 6:6 mbele ya wasio waamini
 2Ko 6:14 Msifungwe nira pamoja na wasio waamini
WASIWASI, Isa 28:16 imani, hatapata wasiwasi
WATAKATIFU, Da 7:18 watakatifu watapeka ule ufalme
WATAWALA, Yoh 12:42 watawala wengi walimwamini
 Mdo 4:26 watawala wakusanyika dhidi ya Yehova
WATENDA DHAMBI, Zb 1:5 watenda dhambi
 Yoh 9:31 Mungu hawasilikizi watenda dhambi
 Ro 5:8 tulipokuwa watenda dhambi Kristo alikuwa
WATENDAJI, Yak 1:22 iweni watendaji wa neno
WATIIFU, Ro 6:17 mmekua watifu kutoka moyoni
WATOTO, Kum 31:12 Wakusanye watu, watoto
 Zb 8:2 Kutoka katika vinywa vya watoto
 Mt 11:16 kama watoto walioketi sokoni
 Mt 18:3 msipogeuika na kuwa kama watoto
 Mt 19:14 Waacheni watoto wadogo waje kwangu
 Lu 10:21 Umeeafunua kwa watoto wadogo
 Ro 8:21 uhuru wenyte utukufu wa watoto wa Mungu
 1Ko 7:14 watoto wenu hawangekuwa safi, lakini sasa
 1Ko 14:20 iweni watoto wadogo kuhusiana na ubaya
 2Ko 12:14 watoto kuwaweeka akiba wazazi
 Efe 6:1 watoto, watini wazazi wenu
 1Yo 3:2 sasa sisi ni watoto wa Mungu
WATUKUFU, 2Pe 2:10 kuwatukana watumkufu
WATUMISHI, Ezr 8:20 watumishi wa hekaluni
 Isa 65:13 Watumishi wangu watakuwa
WATUMISHI WA HUDUMA, 1Ti 3:8 watumishi wa huduma
WATUMWA, Lu 17:10 Sisi ni watumwa wasiofaa kitu
 1Ko 7:23 acheni kuwa watumwa wa wanadamu
WATU WAZIMA, 1Ko 14:20 watu wazima katika uelewaji
WAUME, Efe 5:25 waume, endeleeni kuwependa wake
 Kol 3:18 wake, jitishieni kwa waume zenu
WAVIVU, Ro 12:11 Iweni wenge bidi, msiwe wavivu
WAVUVI WA WATU, Mt 4:19 muwe wavuvi wa watu
WAWU WA KUKOKOTA, Mt 13:47 kama wawu wa kukokota
WAWILI WAWILI, Lu 10:11 wengine 70, wawili wawili
WAYAHUDI, Ro 3:29 ni Mungu wa Wayahudi peke yao?
WAZAZI, Lu 18:29 amecha wazazi kwa ajili ya Ufalme
 Lu 21:16 mtakabidhiwa hata na wazazi
 2Ko 12:14 akiba, wazazi kwa ajili ya watoto wao
 Efe 6:1 watini wazazi wenu
 Kol 3:20 watini wazazi wenu katika kila jambo
WAZAZI WA WAZAZI, 1Ti 5:4 kuwalipa wazazi wa wazazi

WAZEE, Tit 1:5 waweke rasmi wazee
WAZIA, Mwa 18:25 jambo usiloweza kuwazia
WAZIMU, Yoh 10:20 Ana roho mwovu naye ana wazimu
WAZINZI, 1Ko 6:9 wazini hawataurithi Ufalme
WAZITO, Ebr 5:11 mmekuwa wazito wa kusikia
WAZO, Ufu 17:17 miyojo yao kutekeleza wazo lake
WEKA, Zb 31:5 Naiweka roho yangu mikononi mwako
WEMA, Isa 5:20 Ole wanaosema wema ni uovu
WENYE AKILI, Lu 10:21 uwemaficha wenye akili
WEZEKANA, Ayu 42:2 hakuna lisilowezezana kwako
 Mt 19:26 kwa Mungu yote yanawezekana
WEZI, Mt 6:20 mbinguni ambako wezi hawatawajua
 1Ko 6:10 wezi hawataurithi Ufalme wa Mungu
WIMBO, Zb 96:1 Mwimbieni Yehova wimbo mpya
 Zb 98:1 Mwimbieni Yehova wimbo mpya
 Mdo 16:25 Paulo na Sila walimsifu kwa wimbo
WINDA, Law 17:13 akiwinda, amwage damu yake
WINGI, Yoh 10:10 wapate uzima kwa wingi
WINGI ZAIDI, Efe 3:20 kufanya kwa wingi zaidi kupita
WINGU, Ebr 12:1 tuna wingu kubwa la mashahidi
WIVU, Zb 106:16 Walimwonea wivu Musa
 Met 6:34 wivu humfanya mume awake hasira
 Met 14:30 wivu huozesha mifupa
 1Ko 13:4 Upendo hauna wivu
WOGA, Mwa 9:2 wataendelea kuwagoga na kuwahofu
 Ayu 31:34 Je, nimewahi kuogopa umati?
 Isa 44:8 msilemazwe na woga
 Lu 12:4 msiwaogope wale wanaoua mwili
 Lu 21:26 Watu watazimia kwa woga
 2Ti 1:7 Mungu hakutupatia roho ya woga
 1Yo 4:18 Hakuna woga katika upendo
WOKOVU, 2Nya 20:17 simameni tuli, muuone wokovu
 Zb 3:8 Wokovu ni wa Yehova
 Mdo 4:12 hakuna wokovu katika mwingine
 Ro 13:11 sasa wokovu wetu uko karibu zaidi
 Flp 2:12 kuufanya kazi wokovu kwa kutetemeka
 Ufu 7:10 Wokovu unatoka kwa Mungu
WONYESHO, 1Ko 4:9 wonyesho wa hadharani

Y

YAH, Kut 15:2 Nguvu zangu na uwezo wangu ni Yah
 Isa 12:2 Yah Yehova ni nguvu zangu
YAKOBO, Mwa 32:24 akapigana na Yakobo
YAKOBO 1., Lu 6:16 Yuda mwana wa Yakobo
YAKOBO 2., Mdo 12:2 Alimua Yakobo ndugu ya Yohana
YAKOBO 3., Mk 15:40 Maria mama ya Yakobo Mdogo
YAKOBO 4., Mt 13:55 na ndugu zake Yakobo
 Mdo 15:13 Walipomaliza, Yakobo akasema
 1Ko 15:7 alimotokea Yakobo, kisha mitume wote
 Yak 1:1 Yakobo, mtumwa wa Mungu na
YALIYOANDIKWA, Ro 15:4 yaliyoandikwa zamani
 1Ko 4:6 msipite mambo yaliyoandikwa
YANAYOHESHIMIKA, 2Ti 2:20 matumizi yanayoheshimika
YATIMA, Kut 22:22 Msimtese yatima
 Zb 68:5 Baba wa mayatima
YEFTHA, Amu 11:30 Yeftha akaweka nadhiri
YEHOSHAFATI, 2Nya 20:3 Yehoshafati akaogopa
YEHOVA, Kut 3:15 Yehova ndilo jina langu milele
 Kut 5:2 Yehova ni nani? Simjui Yehova kamwe
 Kut 6:3 jina langu Yehova sikujitambulisha
 Kut 20:7 Usilitumie jina Yehova isivyofaa
 Kum 6:5 umpende Yehova kwa moyo wote
 Kum 7:9 Yehova Mungu wa kweli, mwaminifu
 Zb 83:18 jina lako ni Yehova, uliye Juu Zaidi
 Isa 42:8 Mimi ni Yehova. Hilo ndilo jina langu
 Ho 12:5 Yehova Mungu wa majeshi, jina la ukumbusho
 Mal 3:6 mimi ni Yehova; sibandiki
 Mk 12:29 Yehova Mungu ni Yehova mmoja
YENYE FAIDA, 1Ko 6:12 halali, lakini si yenye faida
YEREMIA, Yer 38:6 wakamtupa Yeremia ndani ya tangi
YERUSALEMU, Yos 18:28 Yebusi, yaani, Yerusalemu
 Da 9:25 neno la kujenga upya Yerusalemu
 Mt 23:37 Yerusalemu, Yerusalemu, muuji
 Lu 2:41 walikuwa na desturi ya kwenda Yerusalemu
 Lu 21:20 mtakapoonza Yerusalemu limezingirwa
 Lu 21:24 Yerusalemu litakanyagwa-kanyagwa
 Mdo 5:28 mmejaza Yerusalemu fundisho lenye

Mdo 15:2 mitume na wazee huko Yerusalemu
 Gal 4:26 Yerusalemu la juu liko huru, ndilo mama yetu
 Ebr 12:22 mmekaribia Yerusalemu la mbinguni
 Ufu 3:12 Yerusalemu Jipya linaloshuka kutoka
 Ufu 21:2 Yerusalemu Jipya, likishuka kutoka
YESE, Isa 17:12 Yesu alikuwa na wana wanane
 Isa 11:1 tawite litakuwa kwenye kisiki cha Yesu
YESU, Mt 1:21 utamwita jina Yesu
YEZEBELI, 1Fa 21:23 Mbwa watamia Yezebeli
 Ufu 2:20 unamvumilia yule wanaamke Yezebeli
YOHANA 1., Mt 21:25 Ubatizo wa Yohana, ulitoka wapi?
 Mk 1:9 Yohana akambatiza Yesu katika Yordani
YOHANA 2., Yoh 1:42 Wewe ni Simoni mwana wa Yohana
YOHANA 3., Mt 4:21 Yakobo na Yohana wana wa
YONA, Yon 2:1 Yona akasali ndani ya tumbo la samaki
YONATHANI, Isa 18:3 Yonathani na Daudi, agano
 1Sa 23:16 Yonathani, akamsaidia Daudi kupata nguvu
YORDANI, Yos 3:13 maji ya Yordani yatasimamisha
 2Fa 5:10 ukaoe mara saba katika Yordani
YOSEFU, Mwa 39:23 Yehova alikuwa pamoja na Yosefu
 Lu 4:22 wakiambiana: Huyu ni mwana wa Yosefu
YOSHUA, Kut 33:11 Yoshua mwana wa Nuni, mhudumu
YOSIA, 2Fa 22:1 Yosia alitawala kwa miaka 31
YOTE MNAYOWEZA, 2Pe 3:14 fanyeni yote mnayoweza
YOTE UNAYOWEZA, 2Ti 2:15 Fanya yote unayoweza
YUDA, Mwa 49:10 Fimbo ya ufalme haitaondoka Yuda
 Mt 27:3 Yuda akajuta akarudisha vipande 30
YUMBAYUMBA, 1Fa 18:21 Mtayumbayumba, maoni mwili

Z

ZAA, Mwa 1:28 Zaeni, muwe wengi
 Isa 66:7 Kabla hajawa na uchungu, alizaa
 1Pe 1:3 alituzaa upya kwenye tumaini
ZAKAYO, Lu 19:2 mwanamume aliyetwa Zakayo
ZALIWA, Ayu 14:1 anayezaliwa na mwanamke
 Zb 51:5 Nilizaliwa nikiwa na hatia ya kosa
ZAMA, 1Ti 4:15 Tafakari, zama
ZAMANI, Isa 65:17 mambo ya zamani hayataingia akiini
ZAWADI, Ro 6:23 zawadi ya Mungu, uzima wa milele
 Ro 12:6 tuna zawadi zinazotofautiana
 1Ko 7:7 ana zawadi yake kutoka kwa Mungu
 Efe 4:8 mateka; alitoa wanaume kuwa zawadi
 Yak 1:17 Kila zawadi njema hutoka juu
ZEEKA, Zb 37:25 Nilikuwa kijana lakini sasa nimezeeka
ZEKARIA 1., Lu 11:51 damu ya Abeli mpaka ya Zekaria
ZEKARIA 2., Ezz 5:1 nabii Hagai na nabii Zekaria
ZEKARIA 3., Lu 1:5 kuhani Zekaria wa kikundi cha
ZEU, Mdo 14:12 Wakaanza kumwita Barnaba Zeu
ZIWA, Ufu 19:20 ziwa la moto linalowaka kwa kiberiti
ZIZI, Yoh 10:16 kondoo wengine, si wa zizi hili
ZOEZA, Met 22:6 Mzoee mvulana, hata atakapozeeka
ZUIA, Isa 14:27 ameama nani anayeweza kuliziua
 1Ko 7:35 sisemi ili niwazuie
 2Th 2:6 mnajua kinachunguika
ZUNGUKA, Da 12:4 watazunguka huku na huku, na ujuzi

0-9

12, Mk 3:14 12, ambao aliwaite mitume
24, Ufu 4:4 viti vya ufalme 24 na wazee 24
70, Zb 90:10 Urefu wa maisha ni miaka 70
 Da 9:2 ukiwa wa Yerusalemu, miaka 70
 Da 9:24 majuma 70 yameumliwa
 Lu 10:1 Bwana alichagua 70 akawatuma
77, Mt 18:22 si mpaka mara saba, bali mpaka mara 77
100, Mt 13:8 kuzaa matunda, mara 100 zaidi
 Mt 18:12 ana kondoo 100 na mmoja apotee
 Mk 10:30 atapata mara 100 sasa
300, Amu 7:7 nitawatumia wanaume 300 kuwaokoa
500, 1Ko 15:6 aliwatokea ndugu zaidi ya 500
666, Ufu 13:18 namba yake ni 666
1,000, Ufu 20:2 akamfunga Shetani kwa miaka 1,000
 Ufu 20:4 kutawala na Kristo kwa miaka 1,000
4,000, Mk 8:20 mikate saba kwa wanaume 4,000
5,000, Mt 14:21 walikula wanaume karibu 5,000
144,000, Ufu 7:4 wale waliotwa muhuri, 144,000
 Ufu 14:3 144,000, walionunuliwa kutoka duniani
185,000, 2Fa 19:35 malaika awaua wanaume 185,000

Kamusi ya Maneno ya Biblia

A

Abi. Jina la mwezi wa 5 katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa 11 katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Julai mpaka katikati ya mwezi wa Agosti. Jina la mwezi huo halitajwi katika Biblia; unarejelewa tu kuwa “mwezi wa tano.” (Hes 33:38; Ezr 7:9)—Angalia Nyongeza B15.

Abibu. Jina asilia la mwezi wa kwanza katika kalenda takatifu ya Wayahudi na mwezi wa saba katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Jina hilo linamaanisha “Masuke Mabichi (ya Nafaka)” na mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Machi mpaka katikati ya mwezi wa Aprili. Baada ya Wayahudi kurudi kutoka uhamishoni, mwezi huo uliitwa Nisani. (Kum 16:1)—Angalia Nyongeza B15.

Abiso. Neno hili linatokana na neno la Kigiriki *a'byssos*, linalomaanisha “-enye kina kirefu sana” au “bila mwisho, bila mipaka.” Linatumiwa katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo kumaanisha mahali au hali ya kuwa kifungoni. Linamaanisha pia kaburi lakini lina maana pana zaidi.—Lu 8:31; Ro 10:7; Ufu 20:3.

Adari. Jina la mwezi wa 12 katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa 6 katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Februari mpaka katikati ya mwezi wa Machi. (Est 3:7)—Angalia Nyongeza B15.

Agano. Makubaliano rasmi, au mkataba, kati ya Mungu na wanadamu au kati ya wanadamu wawili ya kufanya au kutofanya jambo fulani. Nyakati fulani ni upande mmoja tu uliokuwa na jukumu la kutekeleza masharti ya agano hilo (agano la upande mmoja ambalo kimsingi lilikuwa ahadi). Nyakati nyingine pande zote mbili zilipaswa kutimiza masharti fulani (agano la pande mbili). Mbali na maagano ambayo Mungu alifanya na wanadamu, Biblia hutaja pia maagano kati ya wanadamu, makabila, mataifa, au vikundi vya watu. Miongoni mwa maagano ambayo yamekuwa na manufaa makubwa sana ni agano ambalo Mungu alifanya na Abrahamu, Daudi, taifa la Israeli (agano la Sheria), na Israeli wa Mungu (agano jipya).—Mwa 9:11; 15:18; 21:27; Kut 24:7; 2Nya 21:7.

Akaya. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, Akaya ni mkoa wa Roma uliokuwa kusini mwa

Ugiriki, na jiji kuu lilikuwa Korintho. Mkoa wa Akaya ulitia ndani eneo lote la Peloponesi na eneo la kati la bara nchini Ugiriki. (Mdo 18:12)—Angalia Nyongeza B13.

Alabasta. Jina la chupa ndogo za manukato ambazo awali zilitengenezwa kwa jiwe lililopatikana karibu na Alabastri, Misri. Kwa kawaida chupa hizo zilitengenezwa zikiwa na shingo nyembamba ambayo ingeweza kuzibwa ili kuzuia manukato hayo yenye thamani yasiyuje. Hatimaye jiwe hilo lilijulikana kwa jina hilo.—Mk 14:3.

Alamothi. Neno la kimuziki linalomaanisha “Wanawali; Wanawake Vijana,” huenda linarejelea sauti za juu (*soprano*) za wanawake vijana. Inaelekea lilitumiwa kuonyesha kwamba muziki ulipaswa kuimbwa au ala ilipaswa kuchezwa kwa sauti ya juu.—1Nya 15:20; Zb 46:Utangulizi.

Alfa na Omega. Ni herufi ya kwanza na herufi ya mwisho katika alfabeti ya Kigiriki; maneno hayo yanatumiwa pamoja mara tatu katika kitabu cha Ufunuo kurejelea cheo cha Mungu. Katika Maandiko hayo, maneno hayo yanamaanisha “wa kwanza na wa mwisho” na “mwanzo na mwisho.”—Ufu 1:8; 21:6; 22:13.

Amina. “Na iwe hivyo,” au “bila shaka.” Neno hili linatokana na shina la Kiebrania *'a-man'*; linalomaanisha “kuwa mwaminifu, kuaminika.” Neno “Amina” lilisemwa ili kukubali kiapo, sala, au taarifa fulani. Katika Ufunuo, linatumiwa likiwa cheo cha Yesu.—Kum 27:26; 1Nya 16:36; Ufu 3:14.

Andiko (Maandiko). Maandishi matakatifu ya Neno la Mungu. Neno hilo linapatikana tu katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.—Lu 24:27; 2Ti 3:16.

Aramu; Waaramu. Wazao wa Aramu mwana wa Shemu ambao waliishi hasa katika maeneo ya Milima ya Lebanoni mpaka Mesopotamia na kuanzia Milima ya Taurusi upande wa kaskazini na kushuka mpaka Damasko na mbele zaidi upande wa kusini. Eneo hilo, linaloitwa Aramu katika Kiebrania, baadaye liliitwa Siria, na wakaaji wake waliitwa Wasiria.—Mwa 25:20; Kum 26:5; Ho 12:12.

Areopago. Kilima kirefu kilicho katika jiji la Athene, upande wa kaskazini magharibi wa Akropoli. Lilikuwa pia jina la baraza au mahakama iliyofanyia mikutano huko. Wanafalsafa Wastoa na Waepikurea walimleta Paulo Areopago ili afaanue mambo aliyoyamini.—Mdo 17:19.

2013

Aselgeia.—Tazama MWENENDO MPOTOVU.

Ashtorethi. Mungu wa kike wa Wakanaani, wa vita na uzazi, mke wa Baali.—1Sa 7:3.

Asia. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, Asia ni jina la mkoa wa Roma ambao ulitia ndani eneo ambalo sasa ni eneo la magharibi nchini Uturuki, na pia visiwa fulani vya pwani, kama vile Samosi na Patmo. Jiji kuu lilikuwa Efeso. (Mdo 20:16; Ufu 1:4)—Angalia Nyongeza B13.

Azazeli. Jina la Kiebrania ambalo huenda linaamaanisha "Mbuzi Anayetoweka." Katika Siku ya Kufunika Dhambi, mbuzi aliyechaguliwa kuwa wa Azazeli alipelekwa na kuachiliwa nyikani, na hivyo kwa njia ya mfano alibeba dhambi za taifa za mwaka uliopita na kwenda nazo.—Law 16:8, 10.

B

Baali. Mungu wa Wakanaani aliyeonwa kuwa mmiliki wa ango na mpaji wa mvua na uzazi. Neno "Baali" lilitumiwa pia kurejelea miungu mingine midogo. Katika Kiebrania neno hilo linamaanisha "Mmiliki; Bwana."—1Fa 18:21; Ro 11:4.

Bathi. Kipimo cha vitu vya majimaji kinachokadiriwa kuwa sawa na lita 22 hivi, kulingana na uchunguzi wa vigae vya kale vya magudulia vilivyokuwa na neno hilo. Katika Biblia, vipimo vingine vingi vikavu na vya vitu vya majimaji vinahesabiwa kulingana na ujazo uliokadiriwa wa kipimo cha bathi. (1Fa 7:38; Eze 45:14)—Angalia Nyongeza B14.

Beelzebubu au Beelzebuli. Jina linalotumiwa kumrejelea Shetani, ambaye ni mkuu, au mtawala, wa roho waovu. Huenda ni Baal-zebubu—jina la Baali aliyebudiwa na Wafilisti kule Ekroni—ambalo limebadilishwa kidogo.—2Fa 1:3; Mt 12:24.

Buli. Jina la mwezi wa nane katika kalenda takatifu ya Wayahudi na jina la mwezi wa pili katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Jina hilo linatokana na neno linalomaanisha "tokeza mazao; zaa" na mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Oktoba mpaka katikati ya mwezi wa Novemba. (1Fa 6:38)—Angalia Nyongeza B15.

C

Chachu. Kitu kilichoongezwa kwenye unga uliokandwa na kwenye vitu vya majimaji ili kuvichachisha; hasa donge lililohifadhiwa la unga uliokandwa na kuchachuka. Mara nyingi chachu hutumiwa katika Biblia kufananisha dhambi na upotovu, hutumiwa pia kurejelea ukuzi unaonea bila kuonekana.—Kut 12:20; Mt 13:33; Gal 5:9.

D

Dagoni. Mungu wa Wafilisti. Chanzo cha neno hili hakijulikani vizuri, lakini baadhi ya wasomi wanalihusianisha na neno la Kiebrania *dagh* (samaki).—Amu 16:23; 1Sa 5:4.

ASELGEIA—DHABIHU YA USHIRIKA

Dariki. Sarafu ya Kiajemi ya dhahabu yenye uzito wa gramu 8.4. (1Nya 29:7)—Angalia Nyongeza B14.

Dekapoli. Kikundi cha majiji ya Kigiriki, ambayo awali yalikuwa majiji kumi (kutokana na neno la Kigiriki *de'ka*, linalomaanisha "kumi," na *po'lis*, linalomaanisha "jiji"). Pia lilikuwa jina la eneo lililokuwa upande wa mashariki wa Bahari ya Galilaya na Mto Yordani, eneo lililokuwa na mengi ya majiji hayo. Majiji hayo yalikuwa vituo vya utamaduni wa Wagiriki na biashara. Yesu alipitia katika eneo hilo, lakini hakuna maandishi yoyote yanayoonyesha kwamba alitembelea mojawapo ya majiji hayo. (Mt 4:25; Mk 5:20)—Angalia Nyongeza A7 na B10.

Dhabihu ya dhambi. Dhambihu iliyotolewa kwa ajili ya dhambi iliyofanywa bila kukusudia kwa sababu ya udhaifu wa mwili usio mkamilifu. Dhambihu za wanyama mbalimbali, kuanzia ng'ombe dume mpaka njwiwa, zilitlewa, kulingana na cheo na hali za yule ambaye dhambi zake zingefunikiwa.—Law 4:27, 29; Ebr 10:8.

Dhambihu ya hatia. Dhambihu za dhambi za mtu binafsi. Ilitofautiana kidogo na dhambihu nyingine za dhambi kwa sababu ilitolewa ili kutimiza au kurudisha haki fulani za agano ambazo mtenda dhambi aliyetubu alikuwa amepoteza kwa sababu ya dhambi na ili kumletea kitalizo kutokana na adhabu.—Law 7:37; 19:22; Isa 53:10.

Dhambihu ya kuteketezwa. Dhambihu ya mnyama aliyeteketezwa juu ya madhabahu na kutolewa kwa Mungu akiwa dhambihu nzima; mwabudu hakuchukua sehemu yoyote ya mnyama huyo (ng'ombe dume, kondoo dume, mbuzi dume, njwiwa tetere, au huwa mchanga).—Kut 29:18; Law 6:9.

Dhambihu ya nadhiri. Ni dhambihu ya hiari iliyombatana na nadhiri fulani.—Law 23:38; 1Sa 1:21.

Dhambihu za shukrani. Ni dhambihu ya ushirika iliyokusudiwa kumsifu Mungu kwa sababu ya maandalizi yake na upendo wake mshikamani-fu. Nyama ya mnyama aliyetolewa dhambihu ililiva pamoja na mikate yenye chachu na mikate isiyo na chachu. Nyama hiyo ilipaswa kuliwa siku hiyohiyo.—2Nya 29:31.

Dhambihu ya ushirika. Dhambihu iliyotolewa kwa Yehova ili kuomba uhusiano wa amani pamoja naye. Mwabudu na watu wa nyumba ni mwake, kuhani aliyehudumu, na makuhani waliokuwa na zamu walishiriki wote kuila. Ni kana kwamba Yehova alipokea moshi unaopendeza wa mafuta yaliyokuwa yakiteketea. Ali-pewa pia damu ambayo huwakilisha uhai. Ni kana kwamba makuhani na waabudu waliketi na kula pamoja na Yehova, kuonyesha kwamba

walikuwa na uhusiano wenye amani.—Law 7:29, 32; Kum 27:7.

Dhabihu. Kitu ambacho mtu anamtotea Mungu ili kumshukuru, kukiri hatia, na kurudisha uhusiano mzuri pamoja naye. Kuanzia Abeli, wanadamu walitoa dhabihu mbalimbali za hiari, kutia ndani wanyama, mpaka agano la Sheria ya Musa lilipofanya kutoa dhabihu hizo kuwa jambo la lazima. Dhabihu za wanyama hazikuhitajika tena Yesu alipotoa uhai wake mwenyewe kuwa dhabihu kamilifu, ingawa Wakristo wanaendelea kumtolea Mungu dhabihu za kiroho.—Mwa 4:4; Ebr 13:15, 16; 1Yo 4:10.

Dhiki kuu. Neno la Kigiriki linalotafsiriwa “dhiki” linatoa wazo la taabu au mateso yanayosababishwa na mikazo inayoletwa na hali. Yesu alizungumza kuhusu “dhiki kuu” isiyo na kifani ambayo ingekumba jiji la Yerusalemu na hasa dhiki ambayo baadaye itawakumba wanadamu ‘atakapokuja akiwa na utukufu’ wakati ujaio. (Mt 24:21, 29-31) Paulo alifafanua kwamba dhiki hiyo ni tendo la uadilifu la Mungu dhidi ya “wale wasiomjua Mungu na wale wasiotii habari nje-ma” kumhusu Yesu Kristo. Kitabu cha Ufunuo sura ya 19 kinaonyesha kwamba Yesu ndiye anayeaongoza majeshi ya mbinguni kupigana na “yule mnyama-mwitu na wafalme wa dunia na majeshi yao.” (2Th 1:6-8; Ufu 19:11-21) “Umati mkubwa” unaonekana ukioleka dhiki hiyo. (Ufu 7:9, 14)—Tazama HAR-MAGEDONI.

Dinari. Sarafu ya fedha ya Kiroma iliyokuwa na uzito wa gramu 3.85 hivi na ilikuwa na picha ya Kaisari upande mmoja. Dinari ilikuwa mshahara wa siku moja wa kibarua na sarafu ya “kodi ya kichwa” ambayo Wayahudi walitozwa na Waroma. (Mt 22:17; Lu 20:24)—Angalia Nyongeza B14.

Drakma. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, neno hili linarejelea sarafu ya fedha ya Kigiriki, ambayo wakati huo ilikuwa na uzito wa gramu 3.4. Maandiko ya Kiebrania yanataja sarafu ya drakma ya dhahabu ya enzi za Waajemi ambayo inalinganishwa na dariki. (Ne 7:70; Mt 17:24)—Angalia Nyongeza B14.

E

Edomu. Jina lingine alilopewa Esau, mwana wa Isaka. Wazao wa Esau (Edomu) walimiliki eneo la Seiri, eneo lenye milima kati ya Bahari ya Chumvi na Ghuba ya ‘Aqaba. Baadaye liliitwa Edomu. (Mwa 25:30; 36:8)—Angalia Nyongeza B3 na B4.

Efa. Kipimo cha vitu vikavu, na pia chombo kilichotumiwa kupimia nafaka. Kilikuwa sawa na kipimo cha bathi cha vitu vya majimaji, kwa hiyo kilikuwa sawa na lita 22. (Kut 16:36; Eze 45:10)—Angalia Nyongeza B14.

Efodi. Vazi linalofanana na kizibao lililovaliwa na makuhani. Kuhani mkuu alivaa efodi ya pekee, na upande wa mbele wa efodi hiyo ulikuwa na kifuko cha kifua kilichokuwa na mawe 12 yenye thamani. (Kut 28:4, 6)—Angalia Nyongeza B5.

Efraimu. Jina la mwana wa pili wa Yosefu; baadaye mojawapo ya makabila ya Israeli liliitwa kwa jina hilo. Baada ya Israeli kugawanyika, Efraimu, ambalo lilikuwa kabila maarufu zaidi, liliwakilisha ufalme wote wa makabila kumi.—Mwa 41:52; Yer 7:15.

Efrati. Mto mrefu zaidi na muhimu zaidi kusi-ni magharibi mwa Asia, na mojawapo ya mito miwili mikubwa Mesopotamia. Unatajwa kwa mara ya kwanza katika Mwanzo 2:14 ukiwa mojawapo ya mito minne ya Edeni. Kwa kawaida unaitwa “ule Mto.” (Mwa 31:21) Ulikuwa mpaka wa kaskazini wa eneo ambalo Waisraeli walipe-wa. (Mwa 15:18; Ufu 16:12)—Angalia Nyongeza B2.

Eluli. Jina la mwezi wa 6 katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa 12 katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Agosti mpaka katikati ya mwezi wa Septemba. (Ne 6:15)—Angalia Nyongeza B15.

Ethanimu. Jina la mwezi wa saba katika kalenda takatifu ya Wayahudi na jina la mwezi wa kwanza katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Septemba mpaka katikati ya mwezi wa Oktoba. Baada ya Wayahudi kurudi kutoka Babiloni, uliitwa Tishri. (1Fa 8:2)—Angalia Nyongeza B15.

Ethiopia. Taifa la kale lililo upande wa kusini wa Misri. Lilitia ndani upande wa kusini kabisa wa nchi ya sasa ya Misri na nchi ambayo sasa inaitwa Sudan. Jina hilo hutumiwa nyakati nyingine badala ya jina “Kushi” la Kiebrania.—Est 1:1.

F

Fadhili zisizostahiliwa. Maneno haya yametafsiriwa kutokana na neno la Kigiriki ambalo wazo lake kuu ni kitu kinachokubalika na kinachopendeza. Mara nyingi neno hilo hutumiwa kurejelea zawadi ya fadhili au utoaji wenye fadhili. Linaorejelea fadhili zisizostahiliwa za Mungu, neno hilo humaanisha zawadi ya bure inayotolewa na Mungu kwa ukarimu, bila kutarajia alipwe chochote. Basi, maneno “fadhili zisizostahiliwa” yanaonyesha jinsi Mungu anavyotoa kwa wingi sana na pia upendo wake mwingi na fadhili zake nyingi sana kuwaelekea wanadamu. Neno la Kigiriki hutafsiriwa pia kwa maneno kama vile “kibali” na “zawadi ya fadhili.” Ni zawadi ambayo mtu hupeva bila kuifanyia kazi na

ambayo hastahili; mtoaji huitoa akichochea tu na ukarimu wake.—2Ko 6:1; Efe 1:7.

Fanya kosa; Kosa. Kufanya kosa ni kukiuka sheria iliyowekwa; kosa ni tendo la ukiukaji wa sheria. Katika Biblia, kosa ni kisawe cha “dhambi.” —Zb 51:3; Ro 5:14.

Farao. Jina la cheo walilopewa wafalme wa Misri. Mafarao watano wanatajwa katika Biblia (Shishaki, So, Tirhaka, Neko, na Hofra), lakini wengine hawatajwi, kutia ndani wale walioshughulika sana na Abrahamu, Musa, na Yosefu.—Kut 15:4; Ro 9:17.

Fidia. Bei inayolipwa ili kumweka mtu huru kutoka katika utakwa, adhabu, mateso, dhambi, au hata wajibu fulani. Bei hiyo haikulipwa kwa pesa tu sikuzote. (Isa 43:3) Fidia ilihitaji kutolewa kwa ajili ya hali mbalimbali. Kwa mfano, wazaliwa wote wa kwanza wa kume au wa wanyama dume walikuwa ya Yehova, na fidia, au bei ya ukombozi, ilihitaji kulipwa ili kuwaweka huru wasihudumu tu katika utumishi wa Yehova. (Hes 3:45, 46; 18:15, 16) Ikiwa ng’ombe dume hatari aliyeachiliwa alimua mtu, mwenye ng’ombe dume huyo alitowza fidia ili kumweka huru kutokana na adhabu ya kifo aliyostahili. (Kut 21:29, 30) Hata hivyo, fidia haikukubaliwa kamwe kwa ajili ya muuaji wa kukusudia. (Hes 35:31) Jambo muhimu zaidi ni kwamba Biblia inakazia fidia ambayo Kristo alilipa kupitia kifo chake cha kidhabihu ili kuwaweka huru wanadamu watiifu kutoka katika dhambi na kifo.—Zb 49:7, 8; Mt 20:28; Efe 1:7.

Finbo ya ufalme. Kirungu au finbo iliyobebwa na mtawala kama ishara ya mamlaka ya kifalme.—Mwa 49:10; Ebr 1:8.

G

Gari la vita. Gari lenye magurudumu mawili lililokotwa na farasi na kutumiwa hasa vitani.—Kut 14:23; Amu 4:13; Mdo 8:28.

Gehena. Neno la Kigiriki linalorejelea Bonde la Hinomu, lililokuwa upande wa kusini na kusini magharibi wa jiji la kale la Yerusalemu. (Yer 7:31) Neno hilo lilitumiwa kinabii kurejelea mahali ambapo maiti zilitupwa. (Yer 7:32; 19:6) Hakuna uthibitisho kwamba wanyama au wanadamu walitupwa katika Gehena ili wateswe au kuchomwa moto wakiwa hai. Kwa hiyo mahali hapo hapangeweza kufananisha mahali pasipoonekana ambapo nafsi za wanadamu zinate-swa milele katika moto halisi. Badala yake, Yesu na wanafunzi wake walitumia neno “Gehena” kufananisha adhabu ya milele ya “kifo cha pili,” yaani, maangamizi ya milele, uharibifu.—Ufu 20:14; Mt 5:22; 10:28.

Gera. Uzito uliolingana na gramu 0.57. Gera moja ilikuwa sehemu 1 ya 20 ya shekeli. (Law 27:25) —Angalia Nyongeza B14.

Gileadi. Lilikuwa hasa eneo lenye rutuba lililokuwa upande wa mashariki wa Mto Yordani, nalo lilifika upande wa kaskazini na upande wa kusini wa Bonde la Yaboki. Nyakati nyingine neno hilo lilitumiwa kurejelea eneo lote la Waisraeli lililokuwa upande wa mashariki wa Yordani, mahali ambapo makabila ya Rubeni, Gadi, na nusu ya kabila la Manase yaliishi. (Hes 32:1; Yos 12:2; 2Fa 10:33)—Angalia Nyongeza B4.

Githithi. Neno la kimuziki ambalo maana yake haijulikani vizuri, ingawa inaonekana kwamba linatokana na neno la Kiebrania *gath*. Baadhi ya watu wanaamini kwamba huenda ni sauti ya muziki inayohusiana na nyimbo zinazommbwa wakati wa kutengeneza divai, kwa sababu neno *gath* linamaanisha shinikizo la divai.—Zb 81:Utangulizi.

H

Habari njema. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo maneno hayo yanarejelea habari njema ya Ufalme wa Mungu na ya wokovu unaotegemea imani katika Yesu Kristo.—Lu 4:18, 43; Mdo 5:42; Ufu 14:6.

Hadesi. Neno la Kigiriki lenye maana sawa na neno la Kiebrania “Sheoli.” Linatafsiriwa kuwa “Kaburi” (kwa herufi kubwa), ili kuonyesha kwamba ni kaburi la wanadamu wote kwa ujumla.—Tazama KABURI.

Har-Magedoni. Neno hili linatokana na neno la Kiebrania *Har Meghid-dohn*, linalomaanisha “Mlima wa Megido.” Neno hilo linahusianishwa na “vita vya siku kuu ya Mungu Mweza-Yote” wakati ambapo “wafalme wa dunia nzima inayokaliwa” watakusanyika kupigana vita dhidi ya Yehova. (Ufu 16:14, 16; 19:11-21)—Tazama DHIKI KUU.

Hekalu. Jengo la kudumu jijini Yerusalemu lililokuwa kitovu cha ibada ya Waisraeli ambalo lilichukua mahali pa hema la ibada lililokuwa likibebwa. Hekalu la kwanza lilijengwa na Sulemani na liliharibiwa na Wababiloni. Hekalu la pili lilijengwa na Zerubabeli baada ya Wayahudi kurudi kutoka uhamishoni Babiloni na baadaye lilijengwa upya na Herode Mkuu. Katika Maandiko, kwa kawaida hekalu linaitwa “nyumba ya Yehova.” (Ezr 1:3; 6:14, 15; 1Nya 29:1; 2Nya 2:4; Mt 24:1)—Angalia Nyongeza B8 na B11.

Hema la ibada. Ni hema la ibada lililoweza kusa-firishwa ambalo lilitumiwa na Waisraeli baada ya Kutoka Misri. Sanduku la agano la Yehova ambalo liliwakilisha uwepo wa Mungu liliwekwa humo, na hema hilo lilikuwa pia mahali pa kutolea dhahibu na kuabudu. Nyakati nyingine linaitwa “hema la mkutano.” Lilijengwa kwa viunzi vya mbao na kufunikwa kwa vitambaa vya kitani vilivyotariziwa kwa michoro ya makerubi. Liligawanywa katika vyumba viwili, kwa kwanza

kilitwa Patakatifu, na cha pili, Patakatifu Zaidi. (Yos 18:1; Kut 25:9)—Angalia Nyongeza B5.

Hema la mkutano. Maneno hayo yanatumiwa kurejelea hema la Musa na pia hema takatifu la ibada ambalo mwanzoni lilipigwa nyikani.—Kut 33:7; 39:32.

Herme. Mungu wa Ugiriki, mwana wa Zeu. Kule Listra, Paulo alitwa kimakosa Herme wakifikiria jukumu ambalo walidhani mungu huyo anatimiza akiwa mjumbe wa miungu na mungu wa ufasaha wa kuzungumza.—Mdo 14:12.

Herode, wafuasi wa chama cha. Wanajulikana pia kuwa Waherode. Waliikuwa wanachama wazalendo waliounga mkono malengo ya kisiasa ya Maherode walipokuwa wakitawala chini ya Waroma. Huenda baadhi ya Masadukayo walikuwa wafuasi wa chama hicho. Waherode walijiunga na Mafarisayo kumpinga Yesu.—Mk 3:6.

Herode. Jina la ukoo la wafalme waliowekwa na Roma ili kuwatawala Wayahudi. Herode Mkuu alijulikana kwa kulijenga upya hekalu la Yerusalemu na kuagiza watoto wachinjwe katika jitihada ya kumwagamiza Yesu. (Mt 2:16; Lu 1:5) Herode Arkelao na Herode Antipa, wana wa Herode Mkuu, waliwewka ili kusimamia maeneo fulani katika milki ya baba yao. (Mt 2:22) Antipa alikuwa mmojawapo wa viongozi wanne wadogo, naye alijulikana kuwa “mfalme” na alitawala wakati wa huduma ya Kristo wa miaka mitatu na nusu kufikia kipindi cha Matendo 12. (Mk 6:14-17; Lu 3:1, 19, 20; 13:31, 32; 23:6-15; Mdo 4:27; 13:1) Kisha, malaika wa Mungu alimua Herode Agripa wa Kwanza, mjukuu wa Herode Mkuu, baada ya kutawala kwa kipindi kifupi. (Mdo 12:1-6, 18-23) Mwanawe, Herode Agripa wa Pili, akawa mtawala, naye alitawala mpaka wakati wa uasi wa Wayahudi dhidi ya Roma.—Mdo 23:35; 25:13, 22-27; 26:1, 2, 19-32.

Higayoni. Neno la kitaalamu la kuongozea muziki. Katika Zaburi 9:16, neno hilo linaweza kumaanisha pumziko katika uimbaji wakati ambapo kinubi kilipigwa kwa sauti nzito ya chini au kituo cha kuwaza kwa uzito kinachomwezesha mtu kutafakari.

Hini. Ni kipimo cha vitu vya majimaji na pia chombo cha kupimia Hini. Ilikuwa sawa na lita 3.67 kulingana na maelezo ya mwanahistoria Yosefo aliyesema kwamba hini ilikuwa sawa na choe mbili za Kiathene. (Kut 29:40)—Angalia Nyongeza B14.

Hisopo. Mmea wenye matawi na majani laini, uliotumiwa kunyunyiza damu au maji kwenye sherehe za kutakasa. Huenda ulikuwa mmea wa *marjoram* (*Origanum maru*; *Origanum syriacum*). Katika Yohana 19:29, huenda ulikuwa mmea wa *marjoram* ulio kwenye tawi au mmea wa dura, aina fulani ya mtama wa kawaida (*Sorghum vulgare*), kwa maana huenda

mmea huo ulikuwa na kijiti kirefu vya kutosha kubeba sifongo ya divai kali na kuifikisha kwenye kinywa cha Yesu.—Kut 12:22; Zb 51:7.

Homeri. Kipimo cha vitu vikavu kinacholingana na kori. Kilikuwa sawa na lita 220, kulingana na ujazo uliokadiriwa wa kipimo cha bathi. (Law 27:16)—Angalia Nyongeza B14.

Horebu; Mlima Horebu. Eneo lenye milima kuzunguka Mlima Sinai. Jina lingine la Mlima Sinai. (Kut 3:1; Kum 5:2)—Angalia Nyongeza B3.

I

Ibilisi. Jina linalomfafanua Shetani katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, linamaanisha “Mchongezi.” Shetani alipewa jina Ibilisi kwa sababu yeye ndiye mchongezi mkuu na wa kwanza kabisa na mshtaki wa uwongo dhidi ya Yehova, neno Lake zuri, na jina Lake takatifu.—Mt 4:1; Yoh 8:44; Ufu 12:9.

Iirikamu. Mkoa wa Roma ulio upande wa kaskazini magharibi wa Ugiriki. Paulo alisafiri mpaka huko katika huduma yake, lakini Biblia haitaji ikiwa alichubiri Iirikamu au alifika tu karibu na mkoa huo. (Ro 15:19)—Angalia Nyongeza B13.

Ishara. Kitu, tendo, hali, au tukio lisilo la kawaida ambalo ni muhimu na ni dalili ya jambo litakalotokea, wakati uliopo au wakati ujao.—Mwa 9:12, 13; 2Fa 20:9; Mt 24:3; Ufu 1:1.

Isiyo na chachu. Maneno haya yanatumiwa kuhusu mikate iliyookwa bila chachu.—Kum 16:3; Mk 14:12; 1Ko 5:8.

Israeli. Jina ambalo Mungu alimpa Yakobo. Baadaye liliwarejelea wazao wake wote kwa ujumla, katika kipindi chochote kile. Kwa kawaida, wazao wa wana 12 wa Yakobo waliitwa wana wa Israeli, nyumba ya Israeli, watu (wanaume) wa Israeli, au Waisraeli. Pia, jina Israeli lilitumiwa kurejelea ufalme wa kaskazini wa makabila kumi ambao ulitengana na ufalme wa kusini, na baadaye lilitumiwa kuwarejelea Wakristo watiwa-mafuta, “Israeli wa Mungu.”—Gal 6:16; Mwa 32:28; 2Sa 7:23; Ro 9:6.

J

Jiji la Daudi. Jiji la Yebusi liliitwa jina hilo baada ya Daudi kulishinda na kujenga makao yake ya kifalme humo. Linaitwa pia Sayuni. Ni sehemu ya kusini mashariki ya Yerusalemu ambayo pia ni ya kale zaidi.—2Sa 5:7; 1NyA 11:4, 5.

Jiwe la kusagia. Jiwe la mvringo lililowekwa juu ya jiwe lingine linalofanana nalo na kutumiwa kusaga nafaka iwe unga. Mchi uliotiwa katikati ya jiwe la chini la kusagia ulishikilia jiwe la juu la kusagia. Katika nyakati za Biblia, mawe ya mkononi ya kusagia yalitumiwa na wanawake katika nyumba nyingi. Kwa kuwa familia ilitegemea jiwe la mkononi la kusagia ili kupata mkate wa kila siku, Sheria ya Musa iliwakataza watu

wasichukue kwa lazima jiwe la chini la kusagia au jiwe la juu kuwa dhamana. Mawe makubwa zaidi ya kusagia yenye muundo huohuo yalizungushwa na wanyama.—Kum 24:6; Mk 9:42.

Jiwe la pembeni. Jiwe linalowekwa kwenye pembe, au kona, ya jengo mahali ambapo kuta mbili zinakutana, lilikuwa muhimu sana katika kuziunganisha na kuzifunga kuta pamoja. Jiwe la msingi la pembeni ndilo lililokuwa jiwe kuu la pembeni; kwa kawaida jiwe ambalo lilikuwa imara lilichaguliwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya umma na kuta za jiji. Neno hilo linatumiwa kwa njia ya mfano kuhusiana na kuwekwa kwa msingi wa dunia, na Yesu anarejelewa kuwa “jiwe la msingi la pembeni” la kutaniko la Kikristo, ambalo linafananishwa na nyumba ya kiroho.—Efe 2:20; Ayu 38:6.

K

Kabi. Kipimo cha vitu vikavu cha lita 1.22, kuliganana na ujazo uliokadiriwa wa kipimo cha bathi. (2Fa 6:25)—Angalia Nyongeza B14.

Kaburi la ukumbusho. Mahali pa kuzikia ambamo mtu aliyekufa aliwekwa. Neno hili linatafsiriwa kutokana na neno la Kigiriki *mne-mei'on*, linalotokana na kitenzi “kukumbusha,” kinachodokeza kwamba mtu aliyekufa anakumbukwa.—Yoh 5:28, 29.

Kaburi. Neno hili linapoanza kwa herufi ndogo, linarejelea kaburi ambamo mtu huzikwa; linapoanza kwa herufi kubwa, linarejelea kaburi la wanadamu kwa ujumla, ambalo katika Kiebrania ni “Sheoli” na katika Kigiriki “Hadesi.” Katika Biblia, linafafanuliwa kuwa mahali pa mfano au hali ambamo mtu awezi kutenda jambo lolote na fahamu zake zote zinakoma.—Mwa 47:30; Mhu 9:10; Mdo 2:31.

Kahaba. Mtu anayefanya ngono nje ya kifungo cha ndoa, hasa ili apate pesa. (Neno la Kigiriki linalotafsiriwa “kahaba,” *por'ne*, linatokana na neno ambalo kimsingi linamaanisha “kuuza.”) Mara nyingi neno kahaba hutumiwa kumhusu mwanamke, ingawa wanaume makahaba wanaatajwa pia katika Biblia. Sheria ya Musa ilikataza ukahaba, na malipo ya kahaba hayakukubaliwa kutolewa kuwa mchango wa mahali patakatifu ya Yehova, tofauti kabisa na zoea la wapagani la kuwatumia makahaba wa hekaluni kuwa chanzo cha mapato. (Kum 23:17, 18; 1Fa 14:24) Biblia hutumia pia neno hilo kwa njia ya mfano, kuwarejelea watu, mataifa, au mashirika yanayojihusisha na aina fulani ya ibada ya sanamu huku yakidai kumwabudu Mungu. Kwa mfano, milki ya kidini inayoitwa “Babiloni Mkubwa” inafafanuliwa katika kitabu cha Ufunuo kuwa kahaba kwa sababu imeshirikiana na watawala wa ulimwengu huu kupata mamlaka na utajiri.—Ufu 17:1-5; 18:3; 1Nya 5:25.

Kaisari. Jina la familia ya Kiroma ambalo lilikuwa kuwa jina la cheo la maliki Waroma. Biblia inawataja Augusto, Tiberio, na Klaudia kwa majina, na ingawa haimtaji Nero kwa jina, yeye pia alikuwa Kaisari. Jina “Kaisari” linatumiwa pia katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo kufananisha mamlaka za kiraia, au Serikali.—Mk 12:17; Mdo 25:12.

Kanaani. Mjukuu wa Noa, na mwana wa nne wa Hamu. Makabila 11 yaliyotokana na Kanaani hatimaye yaliishi katika eneo la mashariki kando ya Mediterania kati ya Misri na Siria. Eneo hilo liliitwa “nchi ya Kanaani.” (Law 18:3; Mwa 9:18; Mdo 13:19)—Angalia Nyongeza B4.

Kemoshi. Mungu mkuu wa Wamoabu.—1Fa 11:33.

Kiapo. Taarifa inayotolewa kwa kuapa ili kuthibitisha kwamba jambo fulani ni la kweli, au ahadi nzito ya kwamba mtu atafanya au hatafanya jambo fulani. Kwa kawaida ni nadhiri inayotolewa kwa mtu mwenye mamlaka, hasa kwa Mungu. Yehova aliliimarisha agano lake pamoja na Abrahamu kwa kiapo.—Mwa 14:22; Ebr 6:16, 17.

Kiaramu. Lugha ya Kiseremiti inayokaribiana sana na Kiebrania, inayotumia alfabeti ya Kiebrania. Awali ilizungumzwa na Waaramu lakini baadaye ikawa lugha ya kimataifa ya biashara na mawasiliano katika milki ya Ashuru na milki ya Babiloni. Pia ilikuwa lugha rasmi ya serikali katika Milki ya Uajemi. (Ezr 4:7) Sehemu fulani za kitabu cha Ezra, Yeremia, na Danieli zilianikwa katika Kiaramu.—Ezr 4:8–6:18; 7:12-26; Yer 10:11; Da 2:4b–7:28.

Kida. Bidhaa hii inatokana na gome la mti wa kida (*Cinnamomum cassia*), ambao uko katika jamii moja na mti wa mdalasini. Kida ilitumiwa kama manukato na kama mojawapo ya viungo vya mafuta matakatifu yaliyotumiwa kutia mafuta.—Kut 30:24; Zb 45:8; Eze 27:19.

Kifuko cha kifua. Kifuko kilichopambwa kwa vito ambacho kilivaliwa na kuhani mkuu wa Israeli juu ya moyo wake wakati wowote aliopinga Patakatifu. Kililitwa “kifuko cha kifua cha maamuzi” kwa sababu kilikuwa na Urimu na Thumimu, vitu ambavyo vilitumiwa kufunua maamuzi ya Yehova. (Kut 28:15-30)—Angalia Nyongeza B5.

Kifuniko cha nguzo. Kilikuwa kifuniko maridadi kilichokuwa juu ya nguzo za hekalu. Nguzo mbili zilizoitwa Yakini na Boazi zilizokuwa upande wa mbele wa hekalu la Sulemani zilikuwa na vifuniko viwili vikubwa. (1Fa 7:16)—Angalia Nyongeza B8.

Kifuniko cha upatanisho. Kifuniko cha sanduku la agano; mbele ya kifuniko hicho kuhani mkuu alinyunyiza damu ya dhambi za dhambi Siku ya Kufunika Dhambi. Kimsingi, neno hilo katika Kiebrania linatokana na kitenzi kinachomaanisha

“kufunika (dhambi)” au labda “kufutilia mbali (dhambi).” Kifuniko hicho chote kilitengenezwa kwa dhahabu, na kilikuwa na makerubi wawili, mmoja upande huu na mwingine upande wa pili. Nyakati nyingine kinaitwa tu “kifuniko.” (Kut 25:17-22; 1Nya 28:11; Ebr 9:5)—Angalia Nyungeza B5.

Kigiriki. Lugha inayozungumzwa na watu wa Ugiriki; mwenyeji wa Ugiriki au mtu ambaye asili ya familia yake ni Ugiriki. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, neno hilo lina maana pana, lina-rejelea watu wote ambao si Wayahudi au watu walioathiriwa na lugha na utamaduni wa Ugiriki.—Yoe 3:6; Yoh 12:20.

Kilemba. Kitambaa kinachovaliwika kwa kuzungushwa kichwani. Kuhani mkuu alivaa kilemba cha kitani bora, kilichokuwa na bamba la dhahabu lililofungwa upande wa mbele kwa uzi wa bluu. Mfalme alivaa kilemba ndani ya taji lake. Ayuba alitumia neno hilo kwa njia ya mfano alipofanishwa haki yake na kilemba.—Kut 28:36, 37; Ayu 29:14; Eze 21:26.

Kilima. Katika Kiebrania, neno “Milo,” linatokana na neno linalomaanisha “jaza.” Septuajinti inatafsiri neno hilo kuwa “ngome.” Inaonekana na kilima hicho kilikuwa sehemu ya kijiografia au sehemu iliyojengwa katika Jiji la Daudi, lakini hajulikani kikamilii kilikuwaje.—2Sa 5:9; 1Fa 11:27.

Kilomita. Kipimo cha umbali kinachotajwa mara moja tu katika maandishi ya awali ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo kwenye Mathayo 5:41, labda kinarejelea maili au kilomita ya Kiroma ambayo ilikuwa sawa na mita 1,479.5 (futi 4,854). Maandiko mengine matau yanayotaja “kilomita,” yaani, Luka 24:13; Yohana 6:19, na Yohana 11:18 yanarejelea kipimo kilichokubalika cha kilomita kilichopatikana kwa kubadilisha kipimo cha kale cha stadia kinachotajwa katika maandishi ya awali.—Angalia Nyungeza B14.

Kiongozi. Linapotumiwa katika Zaburi, inaonekana kwamba neno hilo katika Kiebrania lina-mrejelea mtu ambaye kwa njia fulani alitunga nyimbo na kuongoza uimbaji wa nyimbo hizo, aliwafundisha na kuwazoeza waimbaji Walawi, na hata aliongoza uimbaji katika pindi rasmi. Tafsiri nyingine zinatafsiri neno hilo kuwa “mwiimbaji mkuu” au “kiongozi wa muziki.”—Zb 4: Utangulizi; 5: Utangulizi.

Kiriba cha divai. Chupa ya ngozi iliyotengenezwa kwa ngozi ya mnyama, kama vile mbuzi au kondoo, ambayo ilitumiwa kuweka divai. Divai iliweka katika viriba vipya vya divai, kwa sababu divai inapochacha, hutokeza gesi ya kaboni dioksidi inayosababisha shinikizo kubwa ndani ya chupa hizo za ngozi. Ngozi mpya hupanuka; ngozi ngumu zilizozeeka hupasuka shinikizo linapoongezeka.—Yos 9:4; Mt 9:17.

Kislevu. Jina la mwezi wa tisa katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa tatu katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Novemba mpaka katikati ya mwezi wa Desemba. (Ne 1:1; Zek 7:1)—Angalia Nyungeza B15.

Kitabu cha kukunjwa. Ukurasa mrefu wa ngozi au mafunjo, uliokuwa na maandishi upande mmoja, ambao kwa kawaida ulikunjwa kwenye kijiti. Maandiko yaliandikwa na kunakiliwa katika vitabu vya kukunjwa; vitabu hivyo vilikuwa vikitumiwa kwa ukawaida wakati Biblia ilipokuwa ikiandikwa.—Yer 36:4, 18, 23; Lu 4:17-20; 2Ti 4:13.

Kitabu cha ngozi. Ngozi ya kondoo, mbuzi, au ndama iliyotayarishwa ili itumiwe kama karatasi ya kuandikwa. Ilidumu kwa muda mrefu kuliko mafunjo na ilitumiwa kutengeneza vitabu vya kukunjwa vya Biblia. Huenda vitabu vya ngozi ambavyo Paulo alimwomba Timotheo amletee vilikuwa sehemu fulani za Maandiko ya Kiebrania. Baadhi ya Vitabu ya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi vilikuwa vya ngozi.—2Ti 4:13.

Kiti cha hukumu. Kwa kawaida lilikuwa jukwaa lililoinuliwa ambalo lilikuwa nje; lilikuwa na ngazi, na maofisa walioketi kwenye kiti hicho wangeweza kuuhutubia umati wa watu na kutangaza maamuzi yao. Maneno “kiti cha hukumu cha Mungu” na “kiti cha hukumu cha Kristo” ni maneno ya mfano yanayomaanisha mpango wa Yehova wa kuwahukumu wanadamu.—Ro 14:10; 2Ko 5:10; Yoh 19:13.

Koleo. Vifaa vilivyotengenezwa kwa dhahabu, ambavyo huenda vilifanana na mikasi; vilitumiwa katika hema la ibada na hekaluni kuzima taa.—Kut 37:23.

Komamanga. Tunda lenye umbo la tofaa, ambalo lina uwa au taji upande mmoja. Ndani ya ganda lake gumu kuna punje nyingi ndogo zilizojaa umajimaji, na kila punje ina mbugu ndogo ya rangi ya waridi au nyekundu. Mapambo yenye umbo la komamanga yalipamba upindo wa joho la bluu lisilo na mikono la kuhani mkuu na pia vifuniko vya nguzo zilizoitwa Yakini na Boazi zilizoakuwa mbele ya hekalu.—Kut 28:34; Hes 13:23; 1Fa 7:18.

Kombeo. Mkanda wa ngozi au mkanda uliosukwa wa kano za wanyama, matete, au manyoya ya wanyama. Kwa kawaida jiwe au kitu kilichopaswa kurushwa kiliwekwa katika sehemu pana ya katikati. Mwisho mmoja wa kombeo ulifungiliwa mkononi au kwenye kitanga cha mkono, na mwisho wa pili ulishikwa na kuachiliwa kombeo lilipozungushwa. Mataifa ya kale yalikuwa na wanajeshi waliorusha mawe kwa kombeo.—Amu 20:16; 1Sa 17:50.

Kori. Kipimo cha vitu vikavu na vya majimaji. Kili kuwa sawa na lita 220, kulingana na ujazo uliokadiriwa wa kipimo cha bathi. (1Fa 5:11) —Angalia Nyongeza B14.

Korongo. Bonde au sakafu ya kijito ambayo kwa kawaida huwa kavu isipokuwa katika majira ya mvua; neno hilo linaweza pia kurejelea kijito cheneyewe. Vijito fulani havikukauka kwa sababu maji yake yalitoka katika chemchemi. Katika Maandiko fulani, korongo linaitwa “bonde.” —Mwa 26:19; Hes 34:5; Kum 8:7; 1Fa 18:5; Ayu 6:15.

Kristo. Jina la cheo la Yesu linalotokana na neno la Kigiriki *Khri-stos*; ambalo ni sawa na neno la Kiebrania linalotafsiriwa kuwa “Masih,” au “Mtiwa-Mafuta.” —Mt 1:16; Yoh 1:41.

Kufunga. Kujizuia kula vyakula vya aina yote kwa kipindi fulani. Waisraeli walifunga katika Siku ya Kufunika Dhambi, nyakati za taabu, na walipohitaji mwongozo kutoka kwa Mungu. Wayahudi walikuwa na pindi nne za kufunga kila mwaka ili kukumbuka pindi za misiba katika historia yao. Kufunga si takwa kwa Wakristo. —Ezr 8:21; Isa 58:6; Lu 18:12.

Kufunika dhambi. Katika Maandiko ya Kiebrania, tendo hilo lilihusiana na dhambi zilizotolewa ili kuwawezesha watu wamkaribie Mungu na kumwabudu. Chini ya Sheria ya Musa, dhambi zililolewa, hasa katika Siku ya kila mwaka ya Kufunika Dhambi, ili watu waweze kupatanishwa na Mungu licha ya dhambi za mtu mmoja-mmoja na taifa zima. Dhambi hizo zilifanisha dhambi ya Yesu, ambayo ilifunika kabisa dhambi za wanadamu mara moja kwa wakati wote, na hivyo kuwapa wanadamu nafasi ya kupatanishwa na Yehova. —Law 5:10; 23:28; Kol 1:20; Ebr 9:12.

Kuhani mkuu. Chini ya Sheria ya Musa, alikuwa kuhani mwenye cheo cha juu aliyewawakilisha watu mbele za Mungu na kuwasimamia makuhani wengine. Anaitwa pia “mkuu wa makuhani.” (2Nya 26:20; Ezr 7:5) Ni yeye peke yake aliyeruhusiwa kuingia Patakatifu Zaidi, chumba cha ndani zaidi cha hema la ibada na baadaye chumba cha ndani zaidi cha hekalu. Alifanya hivyo wakati tu wa Siku ya kila mwaka ya Kufunika Dhambi. Maneno “kuhani mkuu” yanatumia pia kumhusu Yesu Kristo. —Law 16:2, 17; 21:10; Mt 26:3; Ebr 4:14.

Kuhani. Mwakilishi rasmi wa Mungu mbele za watu aliowatumikia, naye aliwafundisha kumhusu Mungu na sheria zake. Pia, makuhani waliwawakilisha watu mbele za Mungu, wakitoa dhambi na pia kuwateteta na kuwaombea watu msamaha. Kabla ya kuanzishwa kwa Sheria ya Musa, kichwa cha familia alitumikia akiwa kuhani wa familia yake. Chini ya Sheria ya Musa, wanaume wa familia ya Haruni katika kabila la

Lawi walikuwa makuhani. Wanaume wengine Walawi walikuwa wasaidizi wao. Wakati wa uzinduzi wa agano jipya, taifa la kiroho la Israeli likawa taifa la makuhani, Yesu Kristo akiwa Kuhani Mkuu. —Kut 28:41; Ebr 9:24; Ufu 5:10.

Kuokota masalio. Ni tendo la kukusanya mazao yoyote ambayo wawunaji waliacha kimakusudi au bila kukusudia. Sheria ya Musa iliwaagiza watu wasivune kabisa kingo za mashamba yao wala kuchukua zeituni zote au zabibu zote. Mungu alimpa maskini, mtu anayeteseka, mkaaji mgeni, yatima, na mjane haki ya kuokota masalio yoyote baada ya mavuno. —Ru 2:7.

Kupeleka uhamishoni. Tendo la kumwondoa mtu kwa lazima katika nchi alimozaliwa au katika makao yake, kwa kawaida washindi walitoa agizo hilo. Neno la Kiebrania linamaanisha “kuondoka.” Katika pindi mbili, Waisraeli wengi sana walipeleka uhamishoni. Ufalme wa kaskazini wa makabila kumi ulipeleka uhamishoni na Waashuru, na baadaye ufalme wa kusini wa makabila mawili ulipeleka uhamishoni na Wababiloni. Wahamishwa waliobaki katika pindi zote mbili walirudishwa katika nchi yao chini ya utawala wa Koreshi, mtawala wa Uajemi. —2Fa 17:6; 24:16; Ezr 6:21.

Kupura; Uwanja wa kupuria. Kupura ni kuondoa nafaka katika bua lake na katika makapi; kazi hiyo ilifanya kwenye uwanja wa kupuria. Nafaka ilipurwa kwa mkono kwa kutumia fimbo, au kiasi kikubwa zaidi cha nafaka kilipurwa kwa vifaa vya pekee, kama vile kifaa cha kupuria nafaka au magurudumu ya kupuria yaliyovutwa na wanyama. Vifaa hivyo vilipitishwa juu ya nafaka iliyotandazwa kwenye uwanja wa kupuria, yaani, eneo tamarare la mvingo ambalo kwa kawaida lilikuwa sehemu iliyooinuka iliyopigwa na upepo. —Law 26:5; Isa 41:15; Mt 3:12.

Kura. Vijiwe vya mvingo au vipande vidogo vya mbaao vilivyotumiwa kufanya maamuzi. Vitu hivyo vilitiwa katika mikunjo ya nguo au katika chombo na kutikiswa. Kura iliyoanguka nje au kutolewa humo ndiyo iliyochaguliwa. Kwa kawaida sala zililolewa wakati wa kupigia kura. Neno “kura” linatumia kihalisi na kwa njia ya mfano kumaanisha “sehemu” au “fungu.” —Yos 14:2; Zb 16:5; Met 16:33; Mt 27:35.

Kusanyiko. Kundi la watu waliokusanyika kuitikia mwito. Katika Maandiko ya Kiebrania, mara nyingi neno hili linatumia kuwarejelea watu wa taifa la Israeli waliokusanyika kwa ajili ya she-rehe za kidini au matukio muhimu ya kitaifa. —Kum 16:8; 1Fa 8:5.

Kusemethi. Aina fulani ya ngano ya hali ya chini (*Triticum spelta*), ambayo mbegu yake haiwezi kutenganishwa kwa urahisi na makapi. —Kut 9:32.

Kutaniko. Kikundi cha watu waliokusanyika pamoja kwa kusudi maalumu au kazi fulani. Katika Maandiko ya Kiebrania, kwa ujumla neno hilo linarejelea taifa la Israeli. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, linarejelea kutaniko moja-moja la Wakristo lakini kwa kawaida linarejelea kutaniko la Kikristo kwa ujumla.—1Fa 8:22; Mdo 9:31; Ro 16:5.

Kuvu. Mojawapo ya magonjwa mengi ya mimea yanayosababishwa na ukungu. Imesemwa kwamba ugonjwa wa kuvu unotajwa katika Biblia ni kizimwili (*Puccinia graminis*).—1Fa 8:37.

Kuwapo. Katika baadhi ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, neno hili linarejelea kuwapo kwa Yesu Kristo akiwa mfalme kuanzia wakati alipoweka kuwa Mfalme wa Kimasihi bila kuonekana na kuendelea mpaka katika siku za mwisho za mfumo huu wa mambo. Kuwapo kwa Kristo si tukio la kuja na kisha kuondoka haraka; badala yake, kuwapo kwake kunadumu kwa kipindi kilichowekwa cha wakati.—Mt 24:3.

Kuwasiliana na roho. Imani ya kwamba roho za wanadamu waliokufa huendelea kuishi baada ya mwili kufa na kwamba zinaweza kuwasiliana na watu walio hai, nazo huwasiliana nao, hasa kupitia mtu (anayewasiliana na roho) anayeweza kutumiwa na roho hizo. Neno la Kigiriki linalotafsiriwa kuwa “mazoea ya kuwasiliana na roho” ni *phar-ma-kí-a*, ambalo kihalisi linamaanisha “ulevi wa dawa.” Neno hilo linahusiana na kuwasiliana na roho kwa sababu katika nyakati za kale, dawa zilitumiwa kuleta nguvu za roho waovu ili kufanya ulozhi.—Gal 5:20; Ufu 21:8.

Kuweka mikono juu ya. Mikono iliwekwa juu ya mtu ili kumweka rasmi kwa ajili ya kazi ya pekee au kumchagua apate baraka, maponyo, au zawadi ya roho takatifu. Nyakati nyingine mikono iliwekwa juu ya wanyama kabla hawajatolewa dhahibu.—Kut 29:15; Hes 27:18; Mdo 19:6; 1Ti 5:22.

L

Laana. Kumtisha au kumtakia uovu mtu au kitu. Neno hilo halipaswi kueleweka kuwa matusi au hasira kali. Kwa kawaida laana ni tangazo rasmi la kiapo au la kumtabiria uovu mtu au kitu, na laana hiyo inapotamkwa na Mungu au na mtu aliyepewa mamlaka inakuwa na uzito na nguvu kama unabii.—Mwa 12:3; Hes 22:12; Gal 3:10.

Lawi; Mlawi. Mwana wa tatu wa Yakobo aliyezaliwa na mke wake Lea; pia ni jina la kabila linaloitwa kwa jina lake. Wanawe watatu walianzisha vikundi vitatu vikuu vya Walawi. Nyakati nyingine, neno “Walawi” linarejelea kabila zima, lakini kwa kawaida halitii ndani familia ya kikuhani ya Haruni. Kabila la Lawi halikugawiwa ardhini katika Nchi ya Ahadi lakini lilipewa majiji 48 kati-

ka ardhini ambayo makabila mengine yaligawiwa.—Kum 10:8; 1Nya 6:1; Ebr 7:11.

Lebanoni, safu ya Milima ya. Mojawapo ya safu mbili za milima nchini Lebanoni. Safu ya milima ya Lebanoni iko upande wa magharibi, na safu ya milima iliyo ng'ambo ya milima ya Lebanoni iko upande wa mashariki. Bonde refu lenye rutuba linatenganisha safu hizo mbili. Safu ya milima ya Lebanoni imeinuka juu kana kwamba ni moja kwa moja kutoka kwenye pwani ya Mediterania, na vilele vyake vimeinuka kufikia urefu wa kati ya mita 1,800 na 2,100 (futi 6,000 na 7,000) kwa wastani. Katika nyakati za kale, nchi ya Lebanoni ilifunikwa na miti mirefu sana ya mierezi, na mataifa jirani yaliiona miti hiyo kuwa yenye thamani kubwa sana. (Kum 1:7; Zb 29:6; 92:12)—Angalia Nyongeza B7.

Leptoni. Katika enzi za Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, Leptoni ilikuwa sarafu ndogo zaidi ya Kiyahudi ya shaba au shaba nyekundu. Tafsiri fulani za Biblia zinaita “sarafu ndogo.” (Mk 12:42; Lu 21:2; maelezo ya chini.)—Angalia Nyongeza B14.

Leviathani. Ni mnyama fulani ambaye kwa kawaida inasemekana kwamba anaka majini. Katika Ayubu 3:8 na 41:1, inaonekana ni mamba au mnyama mwingine wa majini ambaye ni mkubwa sana na ana nguvu nyingi. Katika Zaburi 104:26, huenda ni aina fulani ya nyangumi. Katika Maandiko mengine neno hilo linatumwiwa kwa njia ya mfano na halihusiani na mnyama fulani hususa.—Zb 74:14; Isa 27:1.

Liwali (wa Babiloni na Uajemi). Mwakilishi wa mfalme, au gavana wa mkoa, katika milki ya Babiloni na ya Uajemi. Liwali aliwekwa na mfalme kuwa mtawala mkuu.—Ezr 8:36; Da 6:1.

Liwali (wa Roma). Gavana mkuu wa mkoa uliokuwa chini ya usimamizi wa Baraza la Roma. Alikuwa na mamlaka ya kuhukumu na ya kijeshi, na ingawa Baraza la Roma lilikuwa na haki ya kuchunguza matendo yake, alikuwa na mamlaka kubwa sana katika mkoa.—Mdo 13:7; 18:12.

Logi. Kipimo kidogo zaidi cha vitu vya majimaji kinachotajwa katika Biblia. Talmudi ya Wayahudi inasema kwamba logi ni sehemu 1 ya 12 ya hini, basi kwa msingi huo, logi ingekuwa sawa na lita 0.31. (Law 14:10)—Angalia Nyongeza B14.

M

Madhabahu. Sehemu iliyoainuliwa au jukwaa lililotengenezwa kwa udongo, mawe, mawe yaliyochongwa, au mbaio zilizofunikwa kwa chuma; sehemu hiyo ilitumiwa kutoa dhahibu au uvumba wakati wa ibada. Katika chumba cha kwanza cha hema la ibada na cha hekalu, kulikuwa na ‘madhabahu ndogo ya dhahabu’ ya kufukizia uvumba. Ilitengenezwa kwa mbaio zilizofuni-

nikwa kwa dhahabu. 'Madhabahu kubwa zaidi ya shaba' iliyotumiwa kutolea dhahabu za kuteketezwa ilikuwa nje katika uya. (Kut 27:1; 39:38, 39; Mwa 8:20; 1Fa 6:20; 2Nya 4:1; Lu 1:11)—Angalia Nyongeza B5 na B8.

Madhehebu. Kikundi cha watu wanaoifuata imani fulani au kiongozi fulani na walio na mafundisho yao wenyewe. Neno hili linatumia kurejelea vikundi viwili maarufu vya dini ya Kiyahudi, yaani, Mafarisayo na Masadukayo. Watu wasio Wakristo waliuita pia Ukristo "madhehebu" au "madhehebu ya Wanazareti," labda waliwaona kuwa farakano la dini ya Kiyahudi. Hatimaye, madhehebu yalisitawi katika kutaniko la Kikristo; "madhehebu ya Nikolao" yanatajwa kihususa katika kitabu cha Ufunuo.—Mdo 5:17; 15:5; 24:5; 28:22; Ufu 2:6; 2Pe 2:1.

Mafarisayo. Dhehebu maarufu la dini ya Kiyahudi katika karne ya kwanza W.K. Hawakuwa wa uzoa wa kikuhani, lakini waliifuata sana Sheria, hata mambo madogo zaidi ya Sheria, nao waliyakweza mapokeo yaliyopitishwa kwa mdomo na kuyaona kuwa kama Sheria. (Mt 23:23) Walipinga uvutano wowote wa utamaduni wa Ugiriki, na wakiwa wasomi wa Sheria na mapokeo, walikuwa na mamlaka kubwa juu ya watu. (Mt 23:2-6) Baadhi yao walikuwa pia washiriki wa Sanhedrini. Kwa kawaida walipinga Yesu kuhusiana na kushika Sabato, mapokeo, na kwa sababu alishirikiana na watenda dhambi na wakusanya kodi. Baadhi yao walikuja kuwa Wakristo, kutia ndani Sauli wa Tarso.—Mt 9:11; 12:14; Mk 7:5; Lu 6:2; Mdo 26:5.

Mafunjo. Mmea wa majini unaofanana na matete uliotumiwa kutengeneza vikapu, vyombo, na mashua. Ulitumiwa pia kutengeneza karatasi za mafunjo za kuandikwa na vitabu vingi vya kuku-njwa.—Kut 2:3.

Mahakimu. Katika serikali ya Babiloni, mahakimu walikuwa maofisa wa raia katika wilaya za utawala waliojua sheria na walikuwa na kiasi fulani cha mamlaka ya kuhukumu. Katika makoloni ya Roma, mahakimu wa raia walikuwa wasimamizi wa serikali. Majukumu yao yalitia ndani kudumisha utaratibu, kudhibiti matumizi ya fedha, kuwahukumu waliowunja sheria, na kugiza adhabu itekelezwe.—Da 3:2; Mdo 16:20.

Mahalathi. Ni wazi kwamba neno hili ni la kimuziki, nalo linapatikana katika utangulizi wa Zaburi 53 na 88. Huenda linahusiana na kitenzi cha Kiebrania ambacho kimsingi kinamaanisha "kudhoofika; kuwa mgonjwa," na kwa hiyo kitenzi hicho kinadokeza sauti ya simanzi na huzuni ambayo inapatana na mambo ya kuhuzunisha yanayotajwa katika nyimbo hizo mbili.

Mahali pa juu. Mahali pa ibada ambapo kwa kawaida palikuwa juu ya kilima, mlima, au jukwaa lililotengenezwa na watu. Ingawa nyakati nyingine watu walitumia mahali pa juu kumwambua Mungu, mara nyingi panahusianishwa na ibada ya kifapa au miungu ya uwongo.—Hes 33:52; 1Fa 3:2; Yer 19:5.

Mahali patakatifu. Kwa ujumla, ni mahali palipotengwa kwa ajili ya ibada, mahali patakatifu. Hata hivyo, mara nyingi neno hilo linamaanisha hema la ibada au hekalu lililokuwa Yerusalemu. Neno hilo linatumia pia kurejelea makao ya Mungu mbinguni.—Kut 25:8, 9; 2Fa 10:25; 1Nya 28:10; Ufu 11:19.

Majiji ya makimbilio. Majiji ya Walawi ambamo mtu aliyewa bila kukusudia angeweza kukimbia ili asiawe na mtu anayelipiza kisasi cha damu. Majiji sita ya makimbilio, yaliyoenea kotekote katika Nchi ya Ahadi, yalichaguliwa na Musa na baadaye na Yohua, chini ya mwongozo wa Yehova. Baada ya kufika katika jiji la makimbilio, mtu aliyekuwa akikimbia humo aliwaambia kesi yake wazee waliokuwa katika lango la jiji hilo, kisha walimkaribisha humo. Ili kuwazuia watu waliowaua wengine kimakusudi wasiutumie vibaya mpango huo, mtu aliyekimbia usalama katika jiji la makimbilio alipaswa kufika mbele ya waamuzi katika jiji ambamo mauaji yalifanyika ili athibitise kwamba hana hatia ya kuuu kimakusudi. Ili athibitisha kwamba hana hatia, alirudishwa katika jiji la makimbilio, ambamo alipaswa kuishi ndani ya mipaka ya jiji hilo maisha yake yote au mpaka kuhani mkuu alipokufa.—Hes 35:6, 11-15, 22-29; Yos 20:2-8.

Makapi. Maganda yanayotenganishwa na sehemu inayoliwa ya nafaka wakati wa kupura na kupepeta. Makapi hutumiwa katika tamathali za usemi kufananisha kitu kisicho na thamani na kisichotamanika.—Zb 1:4; Mt 3:12.

Makedonia. Eneo lililo upande wa kaskazini wa Ugiriki ambalo lilipata umaarufu wakati wa Aleksanda Mkuu na kuendelea kuwa huru mpaka liliposhindwa na Waroma. Makedonia ilikuwa mkoa wa Roma mtume Paulo alipotembelea Ulaya kwa mara ya kwanza. Paulo alitembelea eneo hilo mara tatu. (Mdo 16:9)—Angalia Nyongeza B13.

Makerubi. Malaika wa cheo cha juu wenye majukumu ya pekee. Wao ni tofauti na maserafi.—Mwa 3:24; Kut 25:20; Isa 37:16; Ebr 9:5.

Malaika mkuu. Maana yake "mkuu wa malaika." Ufafanuzi huo, pamoja na ukweli wa kwamba Biblia inatumia tu hali ya umoja inapomrejelea "malaika mkuu," huthibitisha kwamba kuna malaika mkuu mmoja tu. Biblia inataja jina la huyo malaika mkuu, inamtambulisha kuwa Mikaeli.—Da 12:1; Yud 9; Ufu 7:7.

Malaika. Linatokana na neno la Kiebrania *mal'akh'* na neno la Kigiriki *ag'ge-los*. Maneno yote mawili kihalisi yanamaanisha “mjumbe” lakini yanatafsiriwa kuwa “malaika” yanapowahusu wajumbe wenye miili ya roho. (Mwa 16:7; 32:3; Jak 2:25; Ufu 22:8) Malaika ni viumbe wa roho walio na nguvu, ambao Mungu aliwaumba kabla ya wanadamu. Katika Biblia wanaitwa pia “makumi ya maelfu ya watakatifu,” “wana wa Mungu,” na “nyota za asubuhi.” (Kum 33:2; Ayu 1:6; 38:7) Hawakuumbwa wakiwa na uwezo wa kuzaa malaika wengine lakini waliumbwa mmoja mmoja. Idadi yao inazidi milioni mia moja. (Da 7:10) Biblia inaonyesha kwamba kila malaika ana jina lake na utu wake, hata hivyo wanakataa kwa unyenyekevu kuabudiwa, na wengi hata hukataa kufunua majina yao. (Mwa 32:29; Lu 1:26; Ufu 22:8, 9) Wana vyeo mbalimbali na wamepeva majukumu mbalimbali, kama vile kuhudumu mbele ya kiti cha Ufalme cha Yehova, kupeleka jumbe zake, kuwasaidia watumishi wa Yehova walio duniani, kutekeleza hukumu za Mungu, na kuunga mkono kazi ya kuhubiri habari njema. (2Fa 19:35; Zb 34:7; Lu 1:30, 31; Ufu 5:11; 14:6) Wakati ujao watajiunga na Yesu kupigana vita vya Har–Magedoni.—Ufu 19:14, 15.

Malkamu. Huenda ni sawa na neno Moleki, mungu mkuu wa Waamoni. (Sef 1:5)—Tazama MOLEKI.

Malkia wa Mbinguni. Jina la cheo la mungu wa kike aliyebudiwa na Waisraeli waasi imani katika siku za Yeremia. Baadhi ya watu wanadai kwamba linarejelea mungu wa kike wa Babiloni aliyetwa Ishari (Astarte). Jina la mungu wa kike wa Wasumeri aliyekuwepo awali, Inanna, linamaanisha “Malkia wa Mbinguni.” Hakuhusianishwa tu na mbingu, bali pia alikuwa mungu wa kike wa uzazi. Astarte anaitwa pia “Bimbwa wa Mbinguni” katika maandishi yaliyocho ngwa ya Wamisri.—Yer 44:19.

Mana. Chakula kikuu ambacho Waisraeli walikuwa kila miaka 40 waliyokuwa nyikani. Kiliandaliwa na Yehova. Kilitokea kimuujiza kwenye ardhi chini ya tabaka la umande kila asubuhi isipokuwa siku ya Sabato. Waisraeli walipokiana kwa mara ya kwanza waliulizana, “Ni nini hiki?” au, katika Kiebrania, “*man hu'?*” (Kut 16:13–15, 35) Katika Maandiko mengine, kinaitwa “nafaka ya mbinguni” (Zb 78:24), “mkate kutoka mbinguni” (Zb 105:40), na “mkate wa wenye nguvu” (Zb 78:25). Yesu alirejelea mana kwa njia ya mfano.—Yoh 6:49, 50.

Manemane. Utomvu unaonata wenye manukato unaotokana na vichaka mbalimbali vya miiba au miti midogo ya jamii ya *Commiphora*. Manemane ni mojawapo ya viungo vilivyotumiwa kutengeneza mafuta matakafifu ya kutia mafuta.

ilitumiwa kutia mavazi au vitanda marashi, na iliiongezwa kwenye mafuta yaliyotumiwa kuka nda mwili na mafuta ya kujipaka. Manemane pia ilitumiwa kuitayarisha miili kabla ya kuizika.—Kut 30:23; Met 7:17; Yoh 19:39.

Maombolezo. Huzuni inayoonyesha waziwazi kwa sababu ya kifo au msiba mwingine. Katika nyakati za Biblia, ilikuwa desturi kuomboleza kwa kipindi fulani. Mbali na kulia kwa sauti kubwa, waombolezaji walivaa mavazi ya pekee, walitia majivu kichwani, wakararua mavazi yao, na kujipigapiga kifua. Nyakati nyingine waombolezaji waliolipwa walialikwa mazishini.—Mwa 23:2; Est 4:3; Ufu 21:4.

Marijani. Kitu kigumu kinachofanana na jive kinachofanyizwa na mifupa ya wanyama wadogo wa baharini. Kinapatikana baharini kikiwa na rangi mbalimbali, kama vile nyekundu, nyeupe, na nyeusi. Marijani yalikuwa mengi sana hasa katika Bahari Nyekundu. Katika nyakati za Biblia, marijani yenye rangi nyekundu yalikuwa na thamani kubwa sana na yalitumiwa kutengeneza shanga na mapambo mengine.—Met 8:11.

Masadukayo. Madhehebu maarufu ya dini ya Kiyahudi ambayo washiriki wake walikuwa watu maarufu walio matajiri na makuhani waliokuwa na mamlaka kubwa kuhusiana na utendaji wa hekaluni. Walikataa mapokeo mengi yaliyopitishwa kwa mdomo ambayo yalifuatwa na Mafarisayo na mafundisho mengine ya Kifarisayo. Hawakuamini ufufuo wala kuwepo kwa malaika. Walimpinga Yesu.—Mt 16:1; Mdo 23:8.

Maserafi. Viumbe wa roho waliosimama kuzunguka kiti cha ufalme cha Yehova mbinguni. Neno la Kiebrania *seraphim'* kihalisi linamaanisha “wanaowaka moto.”—Isa 6:2, 6.

Masihi. Neno hili linatokana na neno la Kiebrania linalomaanisha “mtiwa–mafuta” au “aliyetiwa mafuta.” Katika Kigiriki neno hili linatafsiriwa kuwa “Kristo.”—Da 9:25; Yoh 1:41.

Maskili. Ni neno la Kiebrania linalopatikana katika tangulizi za zaburi 13 ambalo maana yake haijulikani vizuri. Huenda linamaanisha “shairi la kutafakari.” Baadhi ya watu wanafikiri kwamba neno sawa na hilo, linalotafsiriwa kuwa “kutumikia kwa busara,” huenda lina maana sawa na neno hilo.—2Nya 30:22; Zb 32:Utangulizi.

Matunda ya kwanza. Mazao ya kwanza kabisa katika majira ya mavuno; kitu kinachopatikana kwanza au malimbuko ya kitu chochote. Yehova alitaka taifa la Israeli limtolee matunda ya kwanza au mazao wa kwanza wa mwanadamu, mnyama, au uzao wa nchi. Wakiwa taifa, Waisraeli walimtolea Mungu matunda ya kwanza wakati wa Sherehe ya Mikate Isiyu na Chachu na wakati wa Pentekoste. Usemi “matunda ya kwanza” ulitumiwa pia kwa njia ya mfano kumrejelea Kristo

na wafuasi wake watiwa-mafuta.—1Ko 15:23; Hes 15:21; Met 3:9; Ufu 14:4.

Mbashiri; Mwaguzi. Mtu anayedai kuwa anaweza kutabiri matukio ya wakati ujao. Makuhani wachawi, wapiga rami, wanajimu, na wengine wanatajwa katika Biblia kuwa wabashiri au waaguzi.—Law 19:31; Kum 18:11; Mdo 16:16.

Mchokoo. Fimbo ndefu yenye ncha kali ya chuma, iliyotumiwa na wakulima kumwongoza mnyama kwa kumdungadunga nayo. Maneno ya mtu mwenye hekima yanayomchochea msikilizaji kutii ushauri wenye hekima yanafananishwa na mchokoo. “Kuipiga teke mchokoo” ni maneno yanayoleta taswira ya ng’ombe dume mkaidi anayekataa kufuata mwongozo wa mchokoo kwa kuipiga teke, na hivyo kujiumiza mwenyewe.—Mdo 26:14; Amu 3:31.

Merodaki. Mungu mkuu wa jiji la Babiloni. Baada ya mfalme wa Babiloni na mtunga sheria Hamurabi kulifanya Babiloni kuwa jiji kuu la Babilonia, umaarufu wa Merodaki (au, Marduki) uliongezeka, na hatimaye akachukua mahali pa miungu kadhaa iliyokuwepo awali, akawa mungu mkuu kati ya miungu yote ya Wababiloni. Baadaye, jina la cheo “Belu” (“Mmiliki”) lilianza kutumiwa badala ya Merodaki (au, Marduki), na kwa kawaida watu walimrejelea Merodaki kwa jina Beli.—Yer 50:2.

Methali. Msemo wa hekima au hadithi fupi inayofundisha somo au kufafanua ukweli muhimu kwa maneno machache sana. Methali ya Biblia inaweza kuwa fumbo au kitendawili. Methali huwasilisha ukweli kwa lugha inayovutia, mara nyingi kupitia mifano. Misemo fulani ilianza kutumiwa kama semi za kuwadhihaki au kuwadharau watu fulani.—Mhu 12:9; 2Pe 2:22.

Mfinyanzi. Mtengenezaji wa vyungu, mabakuli, na vyombo vingine vya udongo. Neno la Kiebrania linalotafsiriwa mfinyanzi kihalisi linamaanisha “anayeumba.” Mara nyingi mamlaka ambayo mfinyanzi anayo juu ya udongo hutumiwa kuonyesha mamlaka ya enzi kuu ambayo Yehova anayo juu watu mmojammoja na mataifa.—Isa 64:8; Ro 9:21.

Mfumo wa (Mifumo ya) mambo. Neno la Kigiriki *ai-on'* hutafsiriwa kwa maneno hayo lina-porejelea hali ya sasa ya mambo au matukio yanayobainisha kipindi fulani cha wakati, enzi, au zama. Biblia hutumia maneno “mfumo wa mambo wa sasa,” kurejelea hali ya sasa ya ulimwengu kwa ujumla na njia ya kilimwengu ya maisha. (2Ti 4:10) Kupitia agano la Sheria, Mungu alianzisha mfumo wa mambo ambao baadhi ya watu wanaweza kuuuta enzi ya Waisraeli au Wayahudi. Kupitia dhabihu yake ya fidia, Yesu Kristo alitumiwa na Mungu kuanzisha mfumo tofauti wa mambo, ambao msingi wake ni kutanukiwa la Wakristo watiwa-mafuta. Huo ulikuwa mwa-

nzo wa enzi mpya, wakati ambapo mambo halisi yaliyokuwa yameonyeshwa mapema katika agano la Sheria yalianza kutimia. Maneno hayo yanapotumiwa katika wingi yanarejelea mifumo mbalimbali ya mambo, au hali mbalimbali zilizopo sasa, ambazo zimekuwapo au zitakazokuwapo.—Mt 24:3; Mk 4:19; Ro 12:2; 1Ko 10:11.

Mgeuzwa imani. Katika Maandiko, neno hili linamaanisha mtu aliyejiunga na dini ya Kiyahudi, na ikiwa ni mwanamume alitahiriwa.—Mt 23:15; Mdo 13:43.

Mikasi ya kukatika tamba za taa. Vifaa vilivyotumiwa katika hema la ibada na hekaluni, ambavyo vilitengenezwa kwa dhahabu au shaba. Huenda vifaa hivyo vilifanana na mikasi na vilitumiwa kukatika tamba za taa.—2Fa 25:14.

Mikatale. Kifaa kilichotumiwa kumfunga mtu ili kumwadhibu. Mikatale fulani ilifunga miguu peke yake, na mengine iliupinda mwili kwa njia inayochosha, labda kwa kufunga miguu, mikono, na shingo.—Yer 20:2; Mdo 16:24.

Mikate ya toleo.—Tazama MIKATE YA WONYESHO.

Mikate ya wonyesho. Mikate 12 iliyowekwa katika safu mbili, mikate sita katika kila safu, kwenye meza katika chumba cha Patakatifu kilichokuwa katika hema la ibada na hekaluni. Inaitwa pia “mikate ya tabaka” na “mikate ya toleo.” Kila siku ya Sabato, mikate hiyo ambayo iliwekwa mbeke za Mungu iliondolewa na mikate mipya kuwekwa kwenye meza hiyo. Kwa kawaida mikate iliyoondolewa ililiwa na makuhani tu. (2Nya 2:4; Mt 12:4; Kut 25:30; Law 24:5-9; Ebr 9:2)—Angalia Nyongeza B5.

Miktamu. Neno la Kiebrania linalotumiwa katika tanguziti sita za zaburi (Zb 16, 56-60). Ni neno la kitaalamu ambalo maana yake haijulikani vizuri, ingawa huenda linahusiana na maneno “maandishi yaliyochongwa.”

Milkomu. Mungu aliyeabudiwa na Waamoni, labda ndiye mungu anayeitwa Moleki. (1Fa 11:5, 7) Sulemani alipokaribia mwisho wa utawala wake alimjengea mungu huyu wa uwongo mahali pa juu.—Tazama MOLEKI.

Mina. Huitwa pia mane katika kitabu cha Ezekieli. Kipimo cha uzito kilichotumika pia kama pesa. Kwa kutegemea uthibitisho wa vitu vya kale unaoonyesha kwamba mina ilikuwa sawa na shekeli 50, na shekeli ilikuwa na uzito wa gramu 11.4, katika Maandiko ya Kiebrania mina ilikuwa na uzito wa gramu 570. Huenda pia kuli-kuwa na mina ya kifalme, kama kulivyokuwa na kipimo cha kifalme cha mkono. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, mina ilikuwa sawa na drakma 100. Ilikuwa sawa na uzito wa gramu 340. Mina 60 zilikuwa sawa na talanta moja. (Ezr 2:69; Lu 19:13)—Angalia Nyongeza B14.

Miujiza; Kazi zenye nguvu. Matendo au matukio yanayozidi nguvu zote zinazojulikana na wanadamu na ambayo yamesababishwa na chanzo kinachozidi uwezo wa wanadamu. Maneno kama vile “ishara,” “dalili,” na “maajabu” hutumiwa nyakati nyingine katika Biblia kumaanisha jambo lilelile.—Kut 4:21; Mdo 4:22; Ebr 2:4.

Mkono. Kipimo cha urefu ambacho kwa wastani kinaanzia kwenye kiwiko mpaka kwenye ncha ya kidole cha kati. Kwa kawaida Waisraeli walitumia kipimo cha mkono chenye urefu wa sentimita 44.5 hivi (inchi 17.5), lakini walitumia pia kipimo cha mkono mrefu zaidi ambacho kilizidi mkono wa kawaida kwa upana wa kitanga cha mkono, sentimita 51.8 hivi (inchi 20.4). (Mwa 6:15; Lu 12:25)—Angalia Nyongeza B14.

Mkristo. Jina ambalo Mungu aliwapa wafuasi wa Yesu Kristo.—Mdo 11:26; 26:28.

Mkuu wa makuhani. Jina lingine la “kuhani mkuu” katika Maandiko ya Kiebrania. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, ni wazi kwamba usemi “wakuu wa makuhani” ulirejelea wanauwe walioongoza katika ukuhani, huenda walitia ndani makuhani wowote wakuu walioondolewa na pia viongozi wa vile vikundi 24 vya makuhani.—2Nya 26:20; Ebr 7:5; Mt 2:4; Mk 8:31.

Mlinzi. Mtu anayewalinda watu au mali kutokana na madhara, kwa kawaida wakati wa usiku, na ambaye anaweza kupiga king’ora aonapo hatari. Kwa kawaida walinzi waliweka juu ya kuta na minara ya jiji ili kuwatazama watu wakiva mbali kabla hawajalikaribia jiji. Mlinzi ambaye ni mwanajeshi huitwa askari mlinzi. Kwa njia ya mfano, manabii walitumikia wakiva walinzi wa taifa la Israeli, walitoa onyo kuhusu uharibifu uliokuwa ukija.—2Fa 9:20; Eze 3:17.

Mlo wa Jioni wa Bwana. Mlo halisi wa mikate isiyona na chachu na divai, vitu ambavyo vinafananishwa mwili wa Kristo na damu yake; navyo ni ukumbusho wa kifo cha Yesu. Kwa kuwa huu ni mwadhimisho ambao Maandiko yanasema Wakristo wanapaswa kuadhimisha, kwa kufaa unaitwa “Ukumbusho.”—1Ko 11:20, 23-26.

Mnadhiri. Linatokana na neno la Kiebrania linaloamaanisha “Aliyetengwa,” “Aliyewekwa Wafu,” “Aliyewekwa Kando.” Kulikuwa na vikundi viwili vya Wanadhiri: wale waliojitolea na wale waliowekwa na Mungu kuwa Wanadhiri. Mwanamume au mwanamke angeweza kuweka nadhiri ya pekee kwa Yehova ili aishi akiwa Mnadhiri kwa kipindi fulani. Wale waliojitolea kuweka nadhiri hiyo walihitaji kuzingatia viziozi vitatu vikuu: hawakupaswa kunyupa kileo chochote wala kula zao lolote la mzabibu, hawakupaswa kunyoka nywele zao, na hawakupaswa kugusa moyoi. Wale waliowekwa na Mungu kuwa Wanadhiri walibaki Wanadhiri maisha yao yote, na Ye-

hova alitaja matakwa hususa waliyopaswa kutii.—Hes 6:2-7; Amu 13:5.

Mnajimu. Mtu anayechunguza mizunguko ya jua, mwezi, na nyota ili atabiri matukio ya wakati ujao.—Da 2:27; Mt 2:1.

Mnazareti. Jina la Yesu, linaloonyesha kwamba alitoka katika mji wa Nazareti. Huenda linaluhusiana na neno la Kiebrania linalotafsiriwa “chipukizi” katika Isaya 11:1. Baadaye neno hilo lilitumiwa pia kuwahusu wafuasi wa Yesu.—Mt 2:23; Mdo 24:5.

Moleki. Mungu wa Waamoni; labda ndiye mungu anayeitwa Malkamu, Milkomu, na Moloki. Huenda ni jina la cheo wala si jina la mungu fulani hususa. Sheria ya Musa ilisema kwamba mtu yeyote aliyewatoa dhahabu watoto wake kwa Moleki alistahili adhabu ya kifo.—Law 20:2; Yer 32:35; Mdo 7:43.

Moloki.—Tazama MOLEKI.

Mpatanishi. Mtu anayeingilia kati ili kuvipatanisha vikundi viwili. Katika Maandiko, Musa ni mpatanishi wa agano la Sheria na Yesu ni mpatanishi wa agano jipya.—Gal 3:19; 1Ti 2:5.

Mpinga-Kristo. Neno la Kigiriki lina maana mbili. Linaelelea chochote ambacho ni *kinyume cha*, au *kinachompinga* Kristo. Linaweza pia kurejelea Kristo wa uwongo, yule *anayechukua nafasi* ya Kristo. Watu wote, mashirika, au vikundi vinaavyodai kwa uwongo kumwakilisha Kristo au vinaavyodai kuwa Masihi au vinavyompinga Kristo na wanafunzi wake vinaweza kwa kufaa kuitwa wapinga-Kristo.—1Yo 2:22.

Mshindio. Katika ufumaji, mshindio ni nyuzi za kitamba zinazotoka kushoto kwenda kulia. Nyuzi hizi zilipita juu na chini ya mtande, yaani, nyuzi ndefu zilizotoka juu kwenda chini.—Law 13:59.

Msimamizi. Ofisa wa cheo cha chini kuliko liwali katika serikali ya Babiloni. Katika Biblia, wasimamizi hawa waliwasimamia watu wenye hekima katika makao ya mfalme wa Babiloni. Wasi-mamizi wanatajwa pia wakati wa utawala wa Mfalme Dario wa Umedii.—Da 2:48; 6:7.

Mtande. Katika ufumaji, mtande ni nyuzi ndefu zinazotoka juu kwenda chini katika kitamba. Nyuzi zinazopita juu na chini ya mtande kutoka kushoto kwenda kulia zinaitwa mshindio.—Amu 16:13.

Mti (Nguzo). Mlingoti ulio wima ambao juu yake mtu aliyeadhibiwa alitundikwa. Ulitumiwa katika mataifa fulani kuwaua watu na/au kuanika maiti ili kuwaonya wengine au kumfedhesha mtu hadharani. Waashuru, waliojulikana kwa sababu ya vita vyao vya vikatili, waliingiza miti yenye ncha kali kwenye tumbo la mateka wao mpaka kifuani na kuiacha miili ya mateka hao ikining’inia juu ya miti hiyo. Hata hivyo, katika Sheria ya Wayahudi, watu waliokuwa na

hatia ya kufanya makosa mazito kama vile kukufuru au kuabudu sanamu waliuawa kwanza kwa kupigwa mawe au kwa njia nyingine, kisha maiti zao zilitundikwa kwenye nguzo, au miti, ili kuwaonya wengine. (Kum 21:22, 23; 2Sa 21:6, 9) Nyakati fulani Waroma waliwafunga tu wakoaji kwenye mti au nguzo, kwa hiyo mkosaji angeishi kwa siku kadhaa na hatimaye kufa kwa sababu ya uchungu, kiu, njaa, na kuchomwa na jua. Nyakati nyingine, kama Yesu alivyouawa, walimtundika mshtakiwa mtini kwa kuipigilia misumari mikono na miguu yake. (Lu 24:20; Yoh 19:14-16; 20:25; Mdo 2:23, 36)—Tazama MTI WA MATESO.

Mti mtakatifu. Neno la Kiebrania (*'ashe-rah'*) linarejelea (1) mlingoti mtakatifu unaomwakilisha Ashera, mungu wa kike wa uzazi wa Wakanaani, au (2) sanamu ya mungu huyo wa kike Ashera. Inaonekana kwamba mlingoti hiyo ilisimama wima na kwa sehemu ilitengenezwa kwa mbao. Huenda zilikuwa nguzo ambazo hazikuwa zimechongwa, au hata miti.—Kum 16:21; Amu 6:26; 1Fa 15:13.

Mti wa mateso. Maneno hayo yametafsiriwa kutokana na neno la Kigiriki *stau-ros'*, linaloanishisha nguzo iliyo wima au mlingoti, kama ule ambao Yesu aliuawa juu yake. Hakuna uthibitisho kwamba neno hilo la Kigiriki lilimaanisha msalaba, kama ule uliotumiwa na wapagani kuwa nembo ya kidini kwa karne nyingi kabla ya Kristo kuja. Maneno "mti wa *mateso*" yanawasilisha maana kamili ya neno la awali, kwa kuwa neno *stau-ros'* linatumiwa pia kurejelea mateso, dhiki, na fedheha ambayo wafuasi wa Yesu wangekabili. (Mt 16:24; Ebr 12:2)—Tazama MTI (NGUZO).

Mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Ni mti uliokuwa katika bustani ya Edeni uliotumiwa na Mungu kuwakilisha haki yake ya kuwawekea wadamu viwango vya "mema" na "mabaya."—Mwa 2:9, 17.

Mti wa uzima. Ni mti uliokuwa katika bustani ya Edeni. Biblia haisemi kwamba kiasili matunda yake yalikuwa na uwezo fulani wa kuendeleza uhai; badala yake, mti huo uliwakilisha uhakikisho wa kwamba Mungu angewapa uzima wa milele wale ambao angewaruhusu kula matunda yake.—Mwa 2:9; 3:22.

Mtu aliye huru; Mtu aliyekwa huru. Wakati wa utawala wa Roma, "mtu aliye huru" ni mtu aliyezaliwa akiwa huru, akiwa na haki kamili za raia. Kinyume chake, "mtu aliyekwa huru" ni mtumwa aliyefunguliwa kutoka utumwani. Mtumwa aliyefunguliwa rasmi kutoka utumwani alipata uraia wa Roma, lakini hakustahili kugombea cheo cha kisiasa. Mtumwa ambaye hakufunguliwa rasmi alipata uhuru lakini hakupata haki kamili za raia.—1Ko 7:22.

Mtu anayewasiliana na roho. Mtu anayedai kwamba anazungumza na watu waliokufa.—Law 20:27; Kum 18:10-12; 2Fa 21:6.

Mtume. Kimsingi neno hili linamaanisha "aliyetumwa," nalo linatumiwa kumhusu Yesu na watu fulani waliotumwa kuwatumikia wengine. Mara nyingi, linatumiwa kuwahusu wanafunzi ambao Yesu mwenyewe aliwachagua wakipa kikundi cha wawakilishi 12 waliowekwa rasmi.—Mk 3:14; Mdo 14:14.

Mtumishi wa huduma. Ni tafsiri ya neno la Kigiriki *di-a'ko-nos*, ambalo mara nyingi hutafsiriwa kuwa "mhudumu" au "mtumishi." "Mtumishi wa huduma" ni yule anayetumikia akiwa msaidizi wa baraza la wazee kutanikoni. Ni lazima atimize viwango vya Biblia ili astahili kupata pendeleo hilo la utumishi.—1Ti 3:8-10, 12.

Muhuri. Kifaa kilichotumiwa kutia alama (kwa kawaida katika udongo wa mfinyanzi au nta), alama ambayo ilionyesha umiliki, uhalisia, au makubaliano. Mihuri ya kale ilitengenezwa kwa kitu kigumu (kama vile jiwe, pembe ya tembo, au ubao) nayo ilikuwa na herufi zilizochoyongwa au michoro iliyoandikwa kurudi nyuma. Muhuri unatumiwa kwa njia ya mfano kurejelea kitu kilichothibitishwa kuwa cha kweli, au kuwa alama ya umiliki, au kitu kilichofichwa au siri.—Kut 28:11; Ne 9:38; Ufu 5:1; 9:4.

Mungu wa kweli. Katika Kiebrania maneno hayo hutafsiriwa kuwa "yule Mungu." Mara nyingi, matumizi ya kibainishi dhahiri katika Kiebrania huonyesha kwamba Yehova peke yake ndiye Mungu wa kweli tofauti na miungu ya uwongo. Maneno "Mungu wa *kweli*" huwasilisha maana kamili kabisa ya maneno hayo ya Kiebrania katika maandiko yenye maneno hayo.—Mwa 5:22, 24; 46:3; Kum 4:39.

Musa, Sheria ya. Sheria ambayo Yehova aliwapa Waisraeli kupitia Musa katika nyika ya Sinai mwaka wa 1513 K.W.K. Kwa kawaida vitabu vya kwanza vitano vya Biblia huitwa Sheria.—Yos 23:6; Lu 24:44.

Muth-labeni. Usemi unaopatikana katika utangulizi wa Zaburi 9. Kulingana na desturi, maana yake ni "kuhusu kifo cha mwana." Baadhi ya watu wanasema kwamba lilikuwa jina au labda maneno ya kwanza ya wimbo uliojulikana ambayo yangetumiwa kuimba zaburi hiyo.

Mwadhimisho wa Miaka 50. Mwadhimisho uliofanywa kila mwaka wa 50, kuanzia wakati ambapo Waisraeli waliingia katika Nchi ya Ahadi. Nchi haikupaswa kulimwa katika mwaka wa Mwadhimisho huo, na watumwa Waebrania walipaswa kuwekwa huru. Ardhi za urithi zilizokuwa zimeuzwa zilirudishwa. Kwa njia fulani, mwaka mzima wa Mwadhimisho huo ulikuwa mwaka wa sherehe, mwaka wa uhuru ambao ulirudisha taifa

katika hali waliyofurahia wakati Mungu alipolia-nzisha taifa hilo mwanzoni.—Law 25:10.

Mwana wa binadamu. Maneno hayo yanapatikana mara 80 hivi katika vitabu vya Injili. Yana-mhusu Yesu Kristo na yanaonyesha kwamba kwa kuzaliwa akiwa na mwili wa nyama, aliku-ja kuwa mwanadamu, wala hakawa kamwe kiu-mbe wa roho aliyejivika mwili wa kibinadamu. Maneno hayo yanaonyesha pia kwamba Yesu angetimiza unabii wa Danieli 7:13 na 14. Katika Maandiko ya Kiebrania, maneno hayo yalitumi-wa kumhusu Ezekieli na Danieli, yakikazia tofau-ti iliyopo kati ya wasemaji hao wanaoweza kufa na Mungu ambaye ni Chanzo cha ujumbe wao.—Eze 3:17; Da 8:17; Mt 19:28; 20:28.

Mwana wa Daudi. Kwa kawaida maneno hayo hutumiwa kumrejelea Yesu, yakikazia kwamba yeye ndiye Mrithi wa agano la Ufalme ambalo li-ngetimizwa na mtu fulani katika ukoo wa Dau-di.—Mt 12:23; 21:9.

Mwandishi. Mtu aliyenakili Maandiko ya Ki-ebrania. Kufikia wakati ambapo Yesu alikuja duniani, neno hilo lilimaanisha watu walioku-wa na ujuzi wa Sheria. Waandishi walimpinga Yesu.—Ezr 7:6, maelezo ya chini; Mk 12:38, 39; 14:1.

Mwangelizi. Mwanamume ambaye jukumu lake la msingi ni kulilinda na kulichunga kutaniko. Wazo kuu la neno la Kigiriki *e-pi'sko-pos* ni kuangalia kwa kusudi la kulinda. Maneno "mwangelizi" na "mzee" (*pre-sby/te-ros*) yanarejelea wadhifa uleule katika kutaniko la Kikristo; neno "mzee" li-naonyesha kwamba mtu aliyewekwa rasmi kuwa mzee ana sifa za ukomavu, na neno "mwangelizi" linakazia majukumu yanayofungamana na wa-dhifa huo.—Mdo 20:28; 1Ti 3:2-7; 1Pe 5:2.

Mwebrania. Neno lililotumiwa mwanzoni kumre-jelea Abramu (Abrahamu), na hivyo kumtofau-tisha na majirani wake Waamori. Baadaye lilitu-miwa kuwahusu wazao wa Abrahamu kupitia Yakobo mjukuu wake na pia lilitumiwa kurejelea lugha yao. Kufikia siku za Yesu, lugha ya Ki-ebrania ilikuwa na maneno mengi ya Kiaramu na ndiyo lugha iliyozungumzwa na Kristo na wa-nafuzi wake.—Mwa 14:13; Kut 5:3; Mdo 26:14.

Mwenendo mpotovu. Usemi huo unatokana na neno la Kigiriki *a-sel'gei-a* ambalo linahusiana na matendo yanayokiuka kabisa sheria za Mun-gu na ambayo yanadhihirisha mtazamo wa ufidhuli au mtazamo unaochukiza usio wa aibu; roho ya kudharau au hata kuchukia mamlaka, sheria, na viwango. Usemi huo haurejelei mwe-nendo usiofaa unaohusu makosa madogo.—Gal 5:19; 2Pe 2:7.

Mwezi mpya. Ni siku ya kwanza ya kila mwe-zi katika kalenda ya Wayahudi, ambayo ilia-dhimishwa ikiwa siku ya kukusanyika pamoja,

kufanya karamu, na kutoa dhabihu za pekee. Baadaye, siku hiyo ilikuja kuwa siku muhimu ya kitaifa ya sherehe, na watu hawakufanya kazi siku hiyo.—Hes 10:10; 2Ny 8:13; Kol 2:16.

Mwonaji. Mtu aliyewezesha na Mungu kutam-bua mapenzi ya Mungu; mtu ambaye ma-cho yake yalifunguliwa ili yaone au kuelewa mambo ambayo wanadamu kwa ujumla hawa-kuona. Neno la Kiebrania linatokana na neno ambalo kimsingi linamaanisha "kuona," iwe ni kihalisi au kwa njia ya mfano. Watu walimfika mwonaji ili kupata ushauri wenye hekima kuhusu matatizo waliyokabili.—1Sa 9:9.

Mwovu au yule Mwovu. Usemi huu hutumiwa ku-mhusu Shtani Ibilisi, anayempinga Mungu na viwango vyake vya uadilifu.—Mt 6:13; 1Yo 5:19.

Myahudi. Neno linalotumiwa kumrejelea mtu wa kabila la Yuda baada ya kuanguka kwa ufalme wa Israeli wa makabila kumi. (2Fa 16:6) Baada ya Waisraeli kutoka uhamishoni Babiloni, lilitu-miwa kuwarejelea Waisraeli wa makabila mba-limbali waliorudi Israeli. (Ezr 4:12) Baadaye, lilitumiwa kotekote ulimwenguni kuwatofauti-sha Waisraeli na watu wasio Waisraeli. (Est 3:6) Mtume Paulo analitumia pia neno hilo kwa njia ya mfano anapofanua kwamba taifa la mtu si muhimu katika kutaniko la Kikristo.—Ro 2:28, 29; Gal 3:28.

Mzaliwa wa kwanza. Neno hilo linamaanisha hasa mtoto mkubwa wa kume wa baba (bada-la ya mtoto wa kwanza anayezaliwa na mama). Katika nyakati za Biblia, mwana mzaliwa wa kwanza aliheshimiwa katika familia, naye ali-pewa jukumu la kuwa kichwa cha familia baba yake alipokufa. Usemi huo unamhusu pia mnyama dume anayezaliwa kwanza.—Kut 11:5; 13:12; Mwa 25:33; Kol 1:15.

Mzee; Mwanamume mzee. Mwanamume mwe-nyye umri mkubwa, lakini katika Maandiko, ma-neno hayo yanarejelea mtu ambaye hasa ana wadhifa wa mamlaka na majukumu katika jamii au taifa. Maneno hayo hutumiwa pia kuwahusu viumbe wa mbinguni katika kitabu cha Ufunuo. Neno la Kigiriki *pre-sby/te-ros* linatafasiirwa kuwa "mzee" linapowarejelea wale walio na jukumu la kuongoza kutanikoni.—Kut 4:29; Met 31:23; 1Ti 5:17; Ufu 4:4.

N

Nabii. Mtu anayetumiwa kutangaza makusudi ya Mungu. Manabii walikuwa wasemaji wa Mungu, hawakutabiri tu bali pia waliwasilisha mafundi-sho ya Yehova, amri zake, na hukumu zake.—Am 3:7; 2Pe 1:21.

Nadhiri. Ahadi takatifu ambayo mtu anamwahi-di Mungu kwamba atafanya jambo fulani, ata-toa dhabihu au zawadi fulani, ataanza utumishi fulani, au atajiepusha na vitu fulani ambavyo kimsingi havijakatazwa. Nadhiri ilikuwa

na uzito kama kiapo.—Hes 6:2; Mhu 5:4; Mt 5:33.

Nafsi. Tafsiri iliyozeleka ya neno la Kiebrania *ne'phesh* na neno la Kigiriki *psy-khe'*. Uchunguzi wa jinsi maneno hayo yanavyotumika katika Biblia, unaonyesha wazi kwamba kimsingi maneno hayo yanamaanisha (1) watu, (2) wanyama, au (3) uhai wa mtu au wa mnyama. (Mwa 1:20; 2:7; Hes 31:28; 1Pe 3:20; pia maelezo ya chini.) Tofauti na jinsi neno "nafsi" linavyotumiwa katika mafundisho mengi ya kidini, Biblia inaonyesha kwamba maneno yote mawili *ne'phesh* na *psy-khe'*, yanapotumiwa kuwahusu viumbe walio duniani, yanarejelea kitu kilicho halisi, kinachoweza kuguswa, kinachoonekana, na kinachoweza kufa. Katika tafsiri hii ya Biblia, mara nyingi maneno hayo ya lugha za awali yametafsiriwa kulingana na maana yake katika kila muktadha, kwa maneno kama vile "uhai," "kiumbe," "mtu," au kama kiwakilishi nafsi (kwa mfano, "mimi" kuwakilisha "nafsi yangu"). Mara nyingi, maelezo ya chini hutaja neno "nafsi" linaloweza pia kutumika. Neno "nafsi" linapotumiwa, katika maandishi makuu au katika maelezo ya chini, linapaswa kueleweka kulingana na ufafanuzi huo. Maneno "kufanya jambo fulani kwa nafsi yote" yanamaanisha kulifanya kwa mwili wote, moyo wote, au kwa uhai wote wa mtu. (Kum 6:5; Mt 22:37) Katika Maandiko mengine, maneno hayo ya lugha za awali yanaweza kutumiwa kumaanisha tamaa au hamu ya kiumbe aliyekufa au maiti.—Hes 6:6; Met 23:2; Isa 56:11; Hag 2:13.

Nardo. Mafuta ghali yenye manukato yaliyokuwa na rangi nyekundu hafifu, yaliyotengenezwa kutokana na mmea wa nardo (*Nardostachys jatamansi*). Kwa kuwa yalikuwa ghali, kwa kawaida mafuta ya nardo yalichanganywa na mafuta mengine yasiyo bora sana, na nyakati nyingine watu walitengeneza mafuta banyaka ya nardo. Haishangazi kwamba Marko na Yohana wanasema kwamba Yesu alimiminiwa "nardo halisi."—Mk 14:3; Yoh 12:3.

Ndoa ya ndugu mkwe. Ni desturi ambayo iliogezwa baadaye katika Sheria ya Musa, iliyo-mruhusu mwanamume kumuoa mjane wa ndugu yake aliyekufa bila mwana ili mwanamume huyo azae watoto na kuendeleza kizazi cha ndugu yake.—Mwa 38:8; Kum 25:5.

Nehilothi. Neno linalopatikana katika utangulizi wa Zaburi ya 5 ambalo maana yake haijulikani vizuri. Baadhi ya watu huamini kwamba linarejelea ala fulani inayopolizwa, nao wanalihusiana neno hilo na neno la Kiebrania ambalo kimsingi linahusiana na neno *cha-lil'* (filimb). Hata hivyo, linaweza kumaanisha sauti ya wimbo.

Nguo za magunia. Zilitengenezwa kwa kitamba kigumu kinachotumiwa kutengenezea magunia, au mifuko, kama ile inayobeba nafaka. Kwa kawaida nguo hizo zilifumwa kwa kutumia manyoya ya mbuzi yaliyokolea rangi, nazo zilikuwa nguo za kitamaduni za maombolezo.—Mwa 37:34; Lu 10:13.

Nguzo takatifu. Nguzo iliyo wima, kwa kawaida ilikuwa ya mawe; ni wazi kwamba ilikuwa sanamu ya uume ya Baali au ya miungu mingine ya uwongo.—Kut 23:24.

Nguzo. Mhimili au mnara au kitu kinachofanana na nguzo. Baadhi ya nguzo zilijengwa ili kuwakumbusha watu mambo au matukio fulani ya kihistoria. Nguzo za kutegemea jengo zilitumiwa katika hekalu na katika majengo mbalimbali ya kifalme yaliyojengwa na Sulemani. Wapagani walisisimamisha nguzo takatifu kwa ajili ya dini yao ya uwongo, na nyakati nyingine Waisraeli waliiga zoea hilo. (Amu 16:29; 1Fa 7:21; 14:23) —Tazama KIFUNIKO CHA NGUZO.

Nira. Kipande cha mti kilichowekwa juu ya mabega ya mtu na mizigo kuning'inizwa kila upande, au ubao au kiunzi kilichowekwa juu ya shingo za wanyama wawili waliovuta mizigo (kwa kawaida ng'ombe); wanyama hao walifungiwa nira walipovuta kifaa cha kulimia au gari la kukokotwa. Kwa kuwa mara nyingi watumwa walitumia nira kubeba mizigo mizito, nira ilitumiwa kwa njia ya mfano kufananisha utumwa au kujitiisha chini ya mtu mwingine, na pia ukandamizaji na mateso. Kuondoa au kuvunja nira kulimaanisha kumweka mtu huru kutoka kifungoni, kutoka katika ukandamizaji, na dhuluma.—Law 26:13; Mt 11:29, 30.

Nisani. Jina jipya la mwezi wa Abibu, mwezi wa kwanza katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa saba katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Machi mpaka katikati ya mwezi wa Aprili. (Ne 2:1)—Angalia Nyongeza B15.

Njia. Usemi huu unatumia kwa njia ya mfano katika Maandiko kumaanisha matendo au mwendo unaokubaliwa au usiokubaliwa na Yehova. Wale waliokuja kuwa wafuasi wa Yesu Kristo waliitwa watu wa "Ile Njia," yaani, waliishi kwa njia iliyotegemea imani katika Yesu Kristo, wakifuata mfano wake.—Mdo 19:9.

Nyara. Vitu vya kibinafsi au vya nyumbani, mifugo, au vitu vingine vyenye thamani vina-vochukuliwa kutoka kwa adui aliyeshindwa.—Yos 7:21; 22:8; Ebr 7:4.

Nyota ya asubuhi.—Tazama NYOTA YA MCHANA.

Nyota ya mchana. Ni sawa na "nyota ya asubuhi." Ndiyo nyota ya mwisho kuchomoza kwenye

upeo wa mashariki kabla ya jua kuchomoza, na hivyo kutangaza kupambazuka kwa siku mpya.—Ufu 22:16; 2Pe 1:19.

Nzige. Jamii mbalimbali za panzi wanaohama katika makundi makubwa. Katika Sheria ya Musa, walionwa kuwa safi na wangeweza kuliwa. Maku-ndi makubwa ya nzige yanayotafuna kila kitu kote yanakopita na kusababisha uharibifu mku-bwa, yalionwa kuwa pigo.—Kut 10:14; Mt 3:4.

O

Omeri. Kipimo cha vitu vikavu kilichokuwa sawa na lita 2.2, au sehemu moja ya kumi ya efa. (Kut 16:16, 18)—Angalia Nyongeza B14.

P

Pakanga. Vijiti vya mimea mbalimbali vyenye la-dha chungu sana na harufu kali inayovutia. Pa-kanga hutumiwa kwa njia ya mfano katika Bib-ليا kufafanua matokeo machungu ya uasherati, utumwa, ukosefu wa haki, na uasi imani. Katika Ufunuo 8:11, “pakanga” humaanisha kitu kichu-ngo chenye sumu, kinachoitwa pia *absinthe*.—Kum 29:18; Met 5:4; Yer 9:15; Am 5:7.

Paradiso. Bustani maridadi, au shamba lililo kama bustani. Paradiso ya kwanza ilikuwa Ede-ni, ambayo Yehova aliwatayarisha wanadamu wawili wa kwanza. Yesu alipokuwa akizungu-mza na mmoja wa wahalifu waliotundikwa kando yake kwenye mti wa mateso, alidokeza kwa-mba dunia itakuwa paradiso. Katika andiko la 2 Wakorintho 12:4, ni wazi kwamba neno hilo li-narejelea paradiso ya wakati ujao, na katika Ufunuo 2:7, linarejelea paradiso ya kimbingu.—Wim 4:13; Lu 23:43.

Pasaka. Sherehe ya kila mwaka iliyofanywa siku ya 14 ya mwezi wa Abibu (baadaye mwezi huo uliitwa Nisani) ili kuadhimisha ukombozi wa Waisraeli kutoka Misri. Iliadhimishwa kwa ku-mchinja na kumchoma mwanakondoo (au mbu-zi), na kumla kwa mboga chungu na mikate isi-yo na chachu.—Kut 12:27; Yoh 6:4; 1Ko 5:7.

Patakatifu Zaidi. Chumba cha ndani zaidi katika hema la ibada na hekaluni, ambamo sanduku la agano liliwekwa; panaitwa pia Patakatifu pa Patakatifu. Kulingana na Sheria ya Musa, ni kuha-ni mkuu peke yake aliyeruhusiwa kuingia Pata-katifu Zaidi, naye angeweza kuingia humo siku moja tu katika Siku ya kila mwaka ya Kufunika Dhambi.—Kut 26:33; Law 16:2, 17; 1Fa 6:16; Ebr 9:3.

Patakatifu. Chumba cha kwanza kikubwa zaidi katika hema la ibada au katika hekalu, nacho ni tofauti na chumba cha ndani zaidi, yaani, Pata-katifu Zaidi. Katika hema la ibada, Patakatifu palikuwa na kinara cha taa cha dhahabu, ma-dhabahu ya uvumba ya dhahabu, meza ya mi-kate ya wonyesho, na vyombo vitakatifu; katika

hekalu, mahali hapo palikuwa na madhabahu ya dhahabu, vinara kumi vya taa vya dhahabu, na meza kumi za mikate ya wonyesho. (Kut 26:33; Ebr 9:2)—Angalia Nyongeza B5 na B8.

Pazia. Kitambaa kilichofumwa kwa njia maridadi na kutariziwa kwa michoro ya makerubi amba-cho kilitenganisha Patakatifu na Patakatifu Zai-di katika hema la ibada na pia hekaluni. (Kut 26:31; 2Nya 3:14; Mt 27:51; Ebr 9:3)—Angalia Nyongeza B5.

Pembe za madhabahu. Sehemu zilizocho-moza kama pembe kwenye kona nne za madhabahu fulani. (Law 8:15; 1Fa 2:28)—Angalia Nyongeza B5 na B8.

Pembe. Neno hili linarejelea pembe za wanyama, ambazo zilitumiwa kama vyombo vya kunywa, vyombo vya mafuta, vyombo vya wino na vipodo-zi, na ala za muziki au za kutoa ishara fulani. (1Sa 16:1, 13; 1Fa 1:39; Eze 9:2) “Pembe” hutu-miwa mara nyingi kwa njia ya mfano kumaani-sha nguvu na ushindi.—Kum 33:17; Mik 4:13; Zek 1:19.

Pentekoste. Sherehe ya pili kati ya sherehe tatu kuu ambazo wanaume wote Wayahudi walipa-swa kusherehekea kule Yerusalemu. Neno Pen-tekoste, linalomaanisha “(Siku) ya Hamsini,” ndilo neno linalotumiwa katika Maandiko ya Ki-giriki ya Kikristo kurejelea Sherehe ya Mavuno au Sherehe ya Majuma inayotajwa katika Ma-andiko ya Kiebrania. Sherehe hiyo ilifanywa siku ya 50 kuanzia Nisani 16.—Kut 23:16; 34:22; Mdo 2:1.

Pete ya muhuri. Aina ya muhuri uliovaliwa kwe-nye kidole au kutiwa kwenye kamba, na huenda ulivaliwa shingoni. Pete hiyo ilikuwa ishara ya mamlaka ya mtawala au ofisa. (Mwa 41:42)—Tazama MUHURI.

Pigo. Katika Maandiko ya Kiebrania, kwa kawaida neno hili linamaanisha tauni, ugonjwa, au adha-bu ya msiba kutoka kwa Yehova. Katika Maandi-ko ya Kigiriki ya Kikristo linamaanisha kupiga kwa kiboko au mjeledi wenye vifundo au ncha kali.—Hes 16:49; Yoh 19:1.

Pima. Kipimo cha urefu kinachotumiwa kupima kina cha maji, ni sawa na mita 1.8 (futi 6). (Mdo 27:28)—Angalia Nyongeza B14.

Pimu. Kipimo cha uzito na pia bei ambayo Wafil-isti walitoza ili kunoa vifaa mbalimbali vya chu-ma. Mawe kadhaa ya kupimia uzito yaliyopati-kana katika machimbo ya vitu vya kale katika nchi ya Israel yana konsonanti za kale za Kiebra-nia za neno “pimu”; kwa wastani yana uzito wa gramu 7.8, ambao ni karibu theluthi mbili za shekeli.—1Sa 13:20, 21.

Porneia.—Tazama UASHERATI.

Purimu. Sherehe ya kila mwaka iliyofanywa siku

ya 14 na ya 15 katika mwezi wa Adari. Inaadhimishwa ili kukumbuka jinsi Wayahudi walivyo-kombolewa ili wasiangamizwe katika siku za Malkia Esta. Neno *pu-rim'* ambalo si la Kiebrania linamaanisha “kura.” Sherehe ya Purimu, au Sherehe ya Kura, iliitwa hivyo kwa sababu ya tendo la Hamani la kupiga Puri (Kura) ili kuamua siku ambayo angetekeza njama yake ya kuwaangamiza Wayahudi.—Est 3:7; 9:26.

R

Rahabu. Jina linalotumiwa kwa njia ya mfano katika kitabu cha Ayubu, Zaburi, na Isaya (si mwanamke Rahabu anayetajwa katika kitabu cha Yohana). Katika kitabu cha Ayubu, mukadha unafunua kwamba huyu Rahabu ni mnyama mkubwa sana wa baharini; katika maandiko mengine mnyama huyu mkubwa sana wa baharini anatumia kufananisha Misri.—Ayu 9:13; Zb 87:4; Isa 30:7; 51:9, 10.

Rehani. Kitu kinachomilikiwa na mkopaji ambacho anampa mkopeshaji ili kumhakikisha kwamba atalipa mkopo. Kitu hicho kiliitwa pia dhama ya mkopo. Sheria ya Musa ilikuwa na maagizo yaliyohusu rehani ambayo yalilinda maskini na raia wa taifa hilo ambao hawakuwa na mtetezi.—Kut 22:26; Eze 18:7.

Roho takatifu. Kani ya utendaji isiyoonekana inayotumiwa na Mungu kutimiza mapenzi yake. Ni takatifu kwa sababu inatoka kwa Yehova, ambaye ni safi na mwadilifu kwa kiwango cha juu zaidi, na kwa sababu ndiyo njia anayotumia Mungu kutimiza mambo matakatifu.—Lu 1:35; Mdo 1:8.

Roho waovu. Viumbe waovu wa roho wasioonekana wenye nguvu zinazozidi za wanadamu. Kwa kuwa wanaitwa “wana wa Mungu wa kweli” katika Mwanzo 6:2 na “malaika” katika Yuda 6, hawakuumbwa wakiwa waovu; badala yake, walikuwa malaika waliojifanya wenyewe kuwa maadui wa Mungu kwa kutomti katika siku za Noa na kujiunga na Shetani katika kumwasi Yehova.—Kum 32:17; Lu 8:30; Mdo 16:16; Yoh 2:19.

Roho. Neno la Kiebrania *ru'ach* na neno la Kigiriki *pneu'ma*, ambayo kwa kawaida hutafsiriwa kuwa “roho” yana maana kadhaa. Yote mawili yanarejelea kitu ambacho macho ya wanadamu hayawezi kuona na huthibitisha kuwapo kwa nguvu inayotenda. Maneno hayo ya Kiebrania na Kigiriki hutumiwa kurejelea (1) upepo, (2) nguvu ya uhai inayotenda ndani ya viumbe walio duniani, (3) nguvu za msukumo zinazotoka katika moyo wa mfano na kumfanya mtu aseme na kutenda mambo kwa njia fulani, (4) maneno yaliyongozwa na roho yanayotoka katika chanzo kichoonekana, (5) Mungu na viumbe

wa roho, na (6) nguvu za utendaji za Mungu, au roho takatifu.—Kut 35:21; Zb 104:29; Mt 12:43; Lu 11:13.

S

Sabato. Neno hili linatokana na neno la Kiebrania linalomaanisha “kupumzika; kukoma.” Ni siku ya saba katika juma la Kiyahudi (ilianza Ijumaa baada ya jua kutua mpaka Jumamosi baada ya jua kutua). Siku nyingine za sherehe katika mwaka ziliitwa pia siku za sabato, kutia ndani mwaka wa 7 na mwaka wa 50. Katika siku ya Sabato, hakuna kazi iliyoipaswa kufanywa isipokuwa utumishi wa makuhani katika mahali patakatifu. Katika miaka ya Sabato, nchi haikupaswa kulimwa na Waebrania hawakupaswa kuwalazimisha Waebrania wenzao walipe madeni. Sheria ya Musa ilikuwa na usawaziko kuhusu mambo yaliyokatazwa siku ya Sabato, lakini viongozi wa kidini waliongeza mambo hayo hatua kwa hatua hivi kwamba kufikia siku za Yesu ilikuwa vigumu kwa watu kuyashika mambo hayo.—Kut 20:8; Law 25:4; Lu 13:14-16; Kol 2:16.

Safi. Katika Biblia, neno hili halimaanishi tu usafi wa kimwili bali pia linamaanisha kudumisha au kurudisha katika hali isiyo na dosari, doa, na kuwa huru kutokana na kitu chochote kinachochafua, kinachotia unajisi, au kupotosha kimaadili au kiroho. Chini ya Sheria ya Musa, neno hilo linamaanisha kuwa safi kisherehe.—Law 10:10; Zb 51:7; Mt 8:2; 1Ko 6:11.

Safu ya Nguzo za Sulemani. Katika siku za Yesu, safu hiyo ilikuwa njia iliyofunikwa upande wa mashariki wa ua wa nje, na wengi waliamini kwamba ilikuwa safu iliyobaki ya hekalu la Sulemani. Yesu alitembea kwenye safu hiyo “wakati wa majira ya baridi kali,” na Wakristo wa mapema walikutana kwenye eneo hilo kwa ajili ya ibada. (Yoh 10:22, 23; Mdo 5:12)—Angalia Nyongeza B11.

Samaria. Kwa miaka 200, lilikuwa jiji kuu la ufalme wa kaskazini wa Israeli wa makabila kumi, na pia lilikuwa jina la eneo lote la makabila hayo. Jiji hilo lilijengwa juu ya mlima uliokuwa na jina hilo. Katika siku za Yesu, Samaria lilikuwa jina la wilaya iliyokuwa kati ya Galilaya upande wa kaskazini na Yudea upande wa kusini. Kwa kawaida Yesu aliepuka kuhubiri katika eneo hilo katika safari zake, lakini nyakati nyingine alipitia humo na kuzungumza na wakaaji wa eneo hilo. Petro alitumia ufunguo wa pili wa mfano wa Ufalme Wasamaria walipopokea roho takatifu. (1Fa 16:24; Yoh 4:7; Mdo 8:14)—Angalia Nyongeza B10.

Sanamu; Ibada ya sanamu. Sanamu ni mfano wa kitu chochote, kitu halisi au cha kuwaziwa, ambacho huenda kikatumiwa na watu katika ibada. Kuabudu sanamu ni kustahi, kupenda,

kuabudu, au kuisujudu sanamu.—Zb 115:4; Mdo 17:16; 1Ko 10:14.

Sanduku la agano. Sanduku lililotengenezwa kwa mbaao za mshita na kufunikwa kwa dhababu, ambalo liliwekwa Patakatifu Zaidi katika hema la ibada na baadaye Patakatifu Zaidi katika hekalu lililolengwa na Sulemani. Liliikuwa na kifuniko cha dhahabu tupu na makerubi wawili walioelekeana. Vitu vya msingi vilivyokuwemo ni yale mabamba mawili yaliyokuwa na zile Amri Kumi. (Kum 31:26; 1Fa 6:19; Ebr 9:4) —Angalia Nyongeza B5 na B8.

Sanhedrini. Mahakama kuu ya Wayahudi iliyokuwa Yerusalemu. Katika siku za Yesu, ilikuwa na washiriki 71, kutia ndani kuhani mkuu na watu wengine ambao awali walikuwa makuhani wakuu, washiriki wa familia za makuhani, wazee, viongozi wa makabila na koo, na waandishi. —Mk 15:1; Mdo 5:34; 23:1, 6.

Sayuni; Mlima Sayuni. Ni jina la jiji la Wayebusi lenye ngome lililoitwa Yebusi ambalo lilikuwa kwenye kilima kilichokuwa upande wa kusini mashariki wa Yerusalemu. Baada ya Daudi kuli-teka, alijenga makao yake ya kifalme huko, na jiji hilo likaanza kuitwa "Jiji la Daudi." (2Sa 5: 7, 9) Mlima Sayuni ukawa mlima mtakatifu hasa kwa Yehova wakati Daudi alipohamisha huko sanduku la agano. Baadaye, jina hilo lililita ndani eno la hekalu kwenye Mlima Moria, na nyakati nyingine jiji lote la Yerusalemu. Mara nyingi jina "Sayuni" hutumiwa kwa njia ya mfano katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.—Zb 2:6; 1Pe 2:6; Ufu 14:1.

Sea. Kipimo cha vitu vikavu. Kulingana na kipimo cha bathi cha ujazo wa vitu vya majimaji, sea ilikuwa sawa na lita 7.33. (2Fa 7:1)—Angalia Nyongeza B14.

Sehemu ya kumi. Sehemu ya kumi, au asilimia 10, iliitolewa au kulipwa ikiwa ushuru, hasa kwa ajili ya makusudi ya kidini. (Mal 3:10; Kum 26:12; Mt 23:23) Chini ya Sheria ya Musa, kila mwaka Walawi walipewa sehemu ya kumi ya mazao ya nchi na sehemu ya kumi ya ongezeko la mifugo ili kuwategemeza. Walawi waliwapa makuhani wa ukoo wa Haruni sehemu ya kumi ya sehemu hiyo ya kumi ili kuwategemeza. Kuli-kuwa pia na sehemu nyingine za kumi. Wakristo hawako chini ya takwa la kutoa sehemu ya kumi.

Sela. Neno la kitaalamu linalohusiana na muziki au kukariri linalopatikana katika kitabu cha Zaburi na Habakuki. Linaweza kumaanisha kituo katika uimbaji au muziki, au mambo yote mawili, kwa kusudi la kutafakari kimyakimya au kuyafanya maneno yaliyotoka kuimbwa yawe wazi. Katika *Septuajinti* ya Kigiriki neno hilo linatafsi-

riwa kuwa *di-a'psal-ma*, linalomaanisha "pumzi-ko la muziki."—Zb 3:4; Hab 3:3.

Shebati. Jina la mwezi wa 11 katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamisho ni Babiloni na jina la mwezi wa 5 katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianza katikati ya mwezi wa Januari mpaka katikati ya mwezi wa Februari. (Zek 1:7)—Angalia Nyongeza B15.

Shekeli. Kipimo cha msingi cha uzito kilichotumiwa na Waebrania na pia kilitumika kama pesa. Kipimo hicho kilikuwa na uzito wa gramu 11.4. Huenda maneno "shekeli ya mahali patakatifu" yalitumiwa kukazia kwamba kipimo hicho kilipaswa kuwa sahihi kabisa au kilipaswa kulingana kabisa na kipimo cha kawaida cha uzito kilichowekwa katika hema la ibada. Huenda kulikuwa na shekeli ya kifalme (iliyokuwa tofauti na shekeli ya kawaida) au kipimo cha kawaida cha uzito kilichowekwa katika makao ya mfalme.—Kut 30:13.

Sheminita. Neno la kimuziki ambalo kihalisi lina-manisha "ya nane" ambayo huenda ni sauti ya chini zaidi au mtindo wa chini. Lilipotumiwa kuhusu ala, huenda neno hilo lilimaanisha ala zilizoata sauti nzito katika muziki. Lilipotumiwa kuhusu nyimbo, inaelekea kwamba lilirejelea ala zilizopigwa kwa sauti nzito za chini zikiambatana na nyimbo zilizoiimbwa kwa sauti hizo. —1Nya 15:21; Zb 6:Utangulizi; 12:Utangulizi.

Sheoli. Neno la Kiebrania lenye maana sawa na neno la Kigiriki "Hadesi." Linatafsiriwa kuwa "Kaburi" (kwa herufi kubwa), ili kuonyesha kwamba ni kaburi la wanadamu wote kwa ujumla wala si kaburi moja.—Mwa 37:35; Zb 16:10; Mdo 2:31 (maelezo ya chini).

Sherehe ya mavuno; Sherehe ya Majuma.—Tazama PENTEKOSTE.

Sherehe ya Mikate Isiyo na Chachu. Sherehe ya kwanza kati ya sherehe tatu kubwa za kila mwaka zilizofanywa na Waisraeli. Ilianza tarehe 15 ya mwezi wa Nisani, siku iliyofuata siku ya Pasaka, na kuendelea kwa siku saba. Ni mikate isiyo na chachu tu iliyopaswa kuliwa, ili kuwakumbusha safari yao ya Kutoka Misri.—Kut 23:15; Mk 14:1.

Sherehe ya Vibanda. Iliitwa pia Sherehe ya Mahe-ma, au Sherehe ya Kukusanya. Ilifanywa tarehe 15-21 ya mwezi wa Ethanimu. Waisraeli walishereheke pindi ya mavuno mwishoni mwa mwaka wa kilimo katika Israeli na ulikuwa wakati wa kushangilia na kushukuru kwa sababu Yehova alibariki mazao yao. Siku za sherehe hiyo, watu walikaa katika vibanda, au mabanda yenyeye umbo la paa, ili kuwakumbusha safari yao ya Kutoka Misri. Ilikuwa kati ya sherehe tatu ambazo wanaume walipaswa kwenda Yerusalemu kuadhimisha.—Law 23:34; Ebr 3:4.

Sherehe ya Wakfu. Ilikuwa sherehe ya kila mwaka ya kukumbuka kutakaswa kwa hekalu baada ya kuchafuliwa na Antioko Epifane. Sherehe hiyo ilianza tarehe 25 ya mwezi wa Kislevu na kuendelea kwa siku nane.—Yoh 10:22.

Sheria. Neno hili linapoandikwa kwa herufi kubwa, mara nyingi linamaanisha Sheria ya Musa au vitabu vya kwanza vitano vya Biblia. Linapoandikwa kwa herufi ndogo, linaweza kumaanisha sheria moja moja katika Sheria ya Musa au kanuni fulani ya sheria.—Hes 15:16; Kum 4:8; Mt 7:12; Gal 3:24.

Shetani. Ni neno la Kiebrania linalomaanisha “Mpinzani.” Neno hilo linapotumiwa na kibainishi dhahiri katika lugha za awali, linamrejelea Shetani Ibilisi, Adui mkuu wa Mungu.—Ayu 1:6; Mt 4:10; Ufu 12:9.

Shinkizo la divai. Kwa kawaida shinkizo la divai lilitengenezwa kwa kuchimba mashimo mawili katika jiwe la chokaa, shimo moja lilikuwa juu kuliko lingine, na mashimo hayo yaliunganishwa kwa mfereji mdogo. Zabibu ziliposhinikizwa katika shimo la juu, maji ya zabibu yalitiririka katika shimo la chini. Maneno hayo yanatumiwa kwa njia ya mfano kurejelea hukumu ya Mungu.—Isa 5:2; Ufu 19:15.

Shohamu. Jiwe lenye thamani ya wastani, aina ngumu ya jiwe la akiki, au jiwe la kalkedoni lenye matabaka mbalimbali. Jiwe la shohamu lina matabaka meupe katikati ya matabaka meusi, ya kahawia, mekundu, ya kijivu, au ya kijani. Jiwe hilo lilitumiwa kwenye mavazi ya pekee ya kuhani mkuu.—Kut 28:9, 12; 1Nya 29:2; Ayu 28:16.

Shubiri. Ni kipimo cha urefu ambacho kwa wastani kinaanzia kwenye ncha ya kidole gumba hadi ncha ya kidole kidogo, kiganja kiwiwa kimepanuliwa. Kwa msingi wa kipimo cha mkono cha sentimita 44.5 (inchi 17.5), shubiri ina urefu wa sentimita 22.2 (inchi 8.75). (Kut 28:16; 1Sa 17:4)—Angalia Nyongeza B14.

Si safi. Usemi huo unaweza kumaanisha kuwa mchafu kimwili au kuvunja sheria za maadili. Hata hivyo, katika Biblia mara nyingi neno hilo linamaanisha kitu kisichokubalika, au kisicho safi, kulingana na Sheria ya Musa. (Law 5:2; 13:45; Mt 10:1; Mdo 10:14; Efe 5:5)—Tazama SAFI.

Siku ya Hukumu. Siku hususa, au kipindi hususa, wakati ambapo vikundi fulani, mataifa, au wanadamu kwa ujumla watawajibika mbele za Mungu. Huenda wakati huo wale watakahukumiwa kuwa wanastahili kifo watauawa, au huenda hukumu hiyo ikawapa baadhi ya watu nafasi ya kuokolewa na kupata uzima wa milele. Yesu Kristo na mitume wake walirejelea “Siku ya Hukumu” inayokuja itakayowahusisha si watu walio hai tu bali pia waliokufa zamani.—Mt 12:36.

Siku ya Kufunika Dhambi. Siku takatifu iliyo muhimu zaidi kwa Waisraeli, inaitwa pia Yom Kippur (maneno hayo yanatokana na neno la Kiebrania *yohm hakk-kip-pur-im*; “siku ya kufunika”), inayofanywa tarehe 10 ya mwezi wa Ethanimu. Ndiyo siku pekee ya mwaka ambayo kuhani mkuu aliingia Patakatifu Zaidi katika hema la ibada na baadaye katika hekalu. Humo alitoka damu ya dhambi kwa ajili ya dhambi zake, dhambi za Walawi wengine, na dhambi za watu wote. Ulikuwa wakati wa kusanyiko takatifu na kufunga, na pia ilikuwa siku ya sabato, wakati ambapo watu hawakupaswa kufanya kazi za kawaida.—Law 23:27, 28.

Siku ya Matayarisho. Jina la siku iliyotangulia Sabato, ambayo ilitumiwa na Wayahudi kufanya matayarisho muhimu. Siku hiyo ilifikia mwisho jua lilipotua siku ambayo leo inaitwa Juma, kisha siku ya Sabato ilianza. Kulingana na Wayahudi, siku ilianza jioni na kufikia mwisho jioni iliyofuata.—Mk 15:42; Lu 23:54.

Siku za mwisho. Maneno haya na mengine yanayofanana nayo, kama vile “kipindi cha mwisho cha zile siku,” yanatumia katika unabii wa Biblia kurejelea wakati ambapo matukio ya kihistoria yatafikia kilele chake. (Eze 38:16; Da 10:14; Mdo 2:17) Ikitegemea unabii unaohusika, huenda kikawa kipindi cha miaka michache tu au mingi. Biblia hasa hutumia maneno hayo kurejelea “siku za mwisho” za mfumo huu wa mambo, wakati wa kuwapo kwa Yesu kusikoonekana.—2Ti 3:1; Yak 5:3; 2Pe 3:3.

Silaha. Vifaa vya kujilinda vilivyovalia na wanajeshi, yaani, kofia, koti la vita, mshipi, vyauma vya kuingia miundi ya miguu, na ngao.—1Sa 31:9; Efe 6:13-17.

Sinagogi. Neno linalomaanisha “kukusanya pamoja; kusanyiko,” lakini katika maandiko mengi, linarejelea jengo au mahali ambapo Wayahudi walikusanyika kwa ajili ya usomaji wa Maandiko, mafundisho, mahubiri, na sala. Katika siku za Yesu, kila mji mkubwa wa Israeli ulikuwa na sinagogi, na majiji makubwa zaidi yalikuwa na masinagogi kadhaa.—Lu 4:16; Mdo 13:14, 15.

Siri takatifu. Sehemu ya kusudi la Mungu ambayo chanzo chake ni Mungu, hubaki ikiwa siri mpaka wakati wa Mungu wa kufunua ufikapo, naye huwafunulia tu wale anaohugua.—Mk 4:11; Kol 1:26.

Siria; Wasiria.—Tazama ARAMU; WAARAMU.

Sirti. Ghuba mbili kubwa zenye kina kifupi zilizo kwenye pwani ya Libya, Afrika Kaskazini, zilizogopwa na mabaharia wa kale kwa sababu zilikuwa na mchanga hatari uliokuwa ukiamishwa hamishwa na mawimbi. (Mdo 27:17)—Angalia Nyongeza B13.

Sivani. Jina la mwezi wa tatu katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa tisa katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianzia katikati ya mwezi wa Mei mpaka katikati ya mwezi wa Juni. (Est 8:9)—Angalia Nyongeza B15.

Suria. Mke wa ziada ambaye kwa kawaida alikuwa kijakazi.—1Fa 21:8; 2Sa 5:13; 1Fa 11:3.

T

Takatifu; Utakatifu. Sifa asilia ya Yehova; hali ya kuwa na usafi kamili kimaadili na utakato. (Kut 28:36; 1Sa 2:2; Met 9:10; Isa 6:3) Linapotumiwa kuwahusu wanadamu (Kut 19:6; 2Fa 4:9); wanyama (Hes 18:17); vitu (Kut 28:38; 30:25; Law 27:14); mahali (Kut 3:5; Isa 27:13); vipindi vya wakati (Kut 16:23; Law 25:12); na kazi (Kut 36:4), neno la awali la Kiebrania huwasilisha wazo la hali ya kutengwa, upekee, au kutakaswa kwa ajili ya Mungu mtakatifu; hali ya kuwekwa kando kwa ajili ya utumishi wa Yehova. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, maneno “takatifu” na “utakatifu” huonyesha pia hali ya kuwekwa kando kwa ajili ya Mungu. Maneno hayo hutumiwa pia kurejelea usafi katika mwendo wa mtu.—Mk 6:20; 2Ko 7:1; 1Pe 1:15, 16.

Talanta. Kipimo kikubwa zaidi cha uzito kilichotumiwa na Waebrania na pia kilitumiwa kama pesa. Kilikuwa na uzito wa kilogramu 34.2. Talanta ya Wagiriki ilikuwa ndogo zaidi, ilikuwa na uzito wa karibu kilogramu 20.4. (1Nya 22:14; Mt 18:24)—Angalia Nyongeza B14.

Tamuzi. (1) Jina la mungu aliyeliwa jijini Yerusalemu na wanawake Waebrania walioasi imani. Inasemekana kwamba mwanzoni Tamuzi alikuwa mfalme ambaye alifanywa kuwa mungu baada ya kifo chake. Katika maandishi ya Wsumeri, Tamuzi anaitwa Dumuzi, naye anatajwa kuwa malkia au mpenzi wa Inanna mungu mke wa uzazi (yaani, Ishtari wa Wababiloni). (Eze 8:14) (2) Jina la mwezi wa nne katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa kumi katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianzia katikati ya mwezi wa Juni mpaka katikati ya mwezi wa Julai.—Angalia Nyongeza B15.

Tanuru. Jiko la kuyeyushia mawe yenye madini au kuyeyushia chuma; hutumiwa pia kuchomea vyombo vya udongo na vyombo vingine vya kauri. Katika nyakati za Biblia, matanuru yalitegemezwa kwa matofali au mawe. Tanuru la kuchomea vyombo vya udongo na vya kauri na chokaa au saruji linaitwa kalibu.—Mwa 15:17; Da 3:17; Ufu 9:2.

Tarshishi, meli za. Mwanzoni neno Tarshishi lilitumiwa kurejelea meli ambazo zilisafiri kwenda katika eneo la kale la Tarshishi (leo ni Hispania).

Inaonekana kwamba hatimaye neno hilo lilirejelea meli kubwa zilizoweza kusafiri mbali. Sulemani na Yehoshafati walitumiwa meli hizo kufanya biashara.—1Fa 9:26; 10:22; 22:48.

Tartaro. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, Tartaro ni hali ya kushushwa hadhi kama ya mfungwa gerezani; malaika walioasi katika siku za Noa walitupwa katika hali hiyo. Kitenzi *tartaro*’o (“kutupa ndani ya Tartaro”) kinachotumiwa katika 2 Petro 2:4 hakimaanishi kwamba “malaika waliofanya dhambi” walitupwa ndani ya Tartaro inayotajwa katika hekaya za wapagani (yaani, gereza lililo chini ya ardhi na mahali penye giza pa miungu midogo). Badala yake, kiteenzi hicho kinaonyesha kwamba Mungu aliwashusha kutoka mahali pao mbinguni na kutoka katika mapendeleo yao na kuwaweka katika hali ya giza zito sana la kiakili kuhusiana na makusudi maingavu ya Mungu. Hatimaye watawekwa katika giza halisi, ambalo Maandiko yanaonyesha kwamba ni maangamizi ya milele, yatakayowapata wao pamoja na mtawala wao, Shetani Ibilisi. Kwa hiyo, Tartaro inafananisha hali ya kushushwa hadhi kabisa ya malaika hao walioasi. Tartaro ni tofauti na “shimo refu lisilo na mwisho” (abiso) linalotajwa katika Ufunuo 20:1-3.

Tarumbeta. Ala inayopulizwa ambayo imetengezwa kwa chuma, nayo hutumiwa kutoa ishara na pia katika muziki. Katika Hesabu 10:2, Yehova alitoa maagizo kwamba tarumbeta mbili za fedha zitengenezwe ili zipigwe kwa miito fulani hususa kwa ajili ya kuwakusanya watu, kuvunja kambi, au kutangaza vita. Inaelekea kwamba tarumbeta hizo hazikuwa zimepinda, tofauti na “ala za pembe” zilizopinda ambazo zilitengenezwa kutokana na pembe za wanyama. Tarumbeta ambazo Biblia haisemi kuhususa jinsi zilivyotengenezwa zilikuwa pia miongoni mwa ala za muziki zilizotumiwa hekaluni. Kwa kawaida sauti za tarumbeta huambatana kwa njia ya mfano na matangazo ya hukumu za Yehova au matukio mengine muhimu ambayo chanzo chake ni Mungu.—2Nya 29:26; Eze 3:10; 1Ko 15:52; Ufu 8:7-11:15.

Tauni au ugonjwa hatari. Ugonjwa wowote wa kuambukiza unaonea kwa kasi ambao unaweza kuathiri wengi na kusababisha vifo. Mara nyingi unahusianishwa na kutekelezwa kwa hukumu ya Mungu.—Hes 14:12; Eze 38:22, 23; Am 4:10.

Tebethi. Jina la mwezi wa kumi katika kalenda takatifu ya Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni Babiloni na jina la mwezi wa nne katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianzia katikati ya mwezi wa Desemba mpaka katikati ya mwezi wa Januari. Kwa kawaida mwezi huo unaitwa “mwezi wa kumi.” (Est 2:16)—Angalia Nyongeza B15.

Terafimu. Miungu ya familia au sanamu, nyakati nyingine ilitumiwa kutafuta ishara za ubashiri. (Eze 21:21) Baadhi ya terafimu zilikuwa na ukubwa na umbo la mwanadamu, na nyingine zilikuwa ndogo. (Mwa 31:34; 1Sa 19:13, 16) Vitu vya kale vilivyopatikana Mesopotamia vinaonyesha kwamba yule aliyekuwa na sanamu za terafimu angepokea urithi wa familia. (Jambo hili linatusaidia kuelewa ni kwa nini Raheli alichukua terafimu za baba yake.) Inaonekana kwamba Waisraeli hawakuwa na desturi hiyo, ingawa hivyo terafimu zilitumiwa katika ibada ya sanamu katika siku za waamuzi na pia wafalme, nazo zilikuwa miongoni mwa vitu vilivyoharibiwa na Mfalme Yosia aliyekuwa mwaminifu.—Amu 17:5; 2Fa 23:24; Ho 3:4.

Tia mafuta. Neno la Kiebrania ambalo kimsingi linamaanisha “kupaka kitu kilicho majimaji.” Mtu au kitu kilipakwa mafuta ili kuonyesha kwamba kimewekwa wakfu kwa ajili ya utumishi wa pekee. Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, neno hilo linatumia kwa kuhusiana na kumimwiwa kwa roho takatifu juu ya wale waliochaguliwa kwa ajili ya tumaini la kwenda mbinguni.—Kut 28:41; 1Sa 16:13; 2Ko 1:21.

Tishiri.—Tazama ETHANIMU na Nyongeza B15.

Toba. Katika Biblia, neno hili hutumiwa kumaanisha kubadili akili na kujuta kutoka moyoni kwa sababu ya njia ya awali ya maisha, matendo ya siyofaa, au kwa sababu ya mambo ambayo mtu alikosa kufanya. Toba ya kweli huzaa matunda, humfanya mtu abadili mwenendo wake.—Mt 3:8; Mdo 3:19; 2Pe 3:9.

Tohara. Tendo la kuondoa govi la kiungo cha kiume. Tohara ilifanywa kuwa takwa kwa Abrahamu na wazao wake, lakini si takwa kwa Wakristo. Neno hilo linatumia kwa njia ya mfano katika maandiko mbalimbali.—Mwa 17:10; 1Ko 7:19; Flp 3:3.

Toleo la kinywaji. Toleo la divai lililomimwa kwenye madhabahu na kutolewa pamoja na nyingi ya zile dhabihu nyingine. Paulo anatumia maneno hayo kwa njia ya mfano kuonyesha utayari wake wa kujitoa kabisa kwa ajili ya Wakristo wenzake.—Hes 15:5, 7; Flp 2:17.

Toleo la kutikiswa. Katika toleo hili inaonekana kwamba kuhani aliweka mikono yake chini ya mikono ya mwabudu aliyekuwa amebeba dhabihu iliyopaswa kutolewa, kisha kuhani aliitiki-sa mikono ya mwabudu huyo kwenda mbele na nyuma; au kuhani mwenyewe alilitiki-sa toleo hilo. Kwa kufanya hivyo ni kana kwamba wali-kuwa *wakimtolea* Yehova matoleo ya dhabihu.—Law 7:30.

Towashi. Kihalisi neno hilo linamaanisha mwanamume aliyehasiwa. Kwa kawaida wanaume hao waliwekwa katika makao ya wafalme ili wawe watumishi au watunzaji wa malkia na masuria.

Neno hilo pia linamrejlea mwanamume ambaye kihalisi hakuwa towashi, bali alikuwa ofisa aliyepewa majukumu mbalimbali katika makao ya mfalme. Linatumia kwa njia ya mfano kumrejlea ‘towashi kwa ajili ya Ufalme,’ mtu ambaye anajidhibiti ili ajitoe kikamili zaidi katika utumishi wa Mungu.—Mt 19:12; Est 2:15; Mdo 8:27.

U

Ua. Eneo lililokuwa wazi kuzunguka hema la ibada na ambalo lilikuwa na uzio; baadaye ua huo ulirejelea mojawapo ya maeneo yaliyokuwa wazi yenye kuta yaliyozunguka jengo kuu la hekalu. Madhabahu ya dhabihu za kuteketezwa ilikuwa katika ua wa hema la ibada na katika ua wa ndani wa hekalu. (Angalia Nyongeza B5, B8, B11.) Biblia inataja pia nyua inapozungumzia nyumba za watu na majumba ya wafalme.—Kut 8:13; 27:9; 1Fa 7:12; Est 4:11; Mt 26:3.

Uadilifu. Katika Maandiko, uadilifu ni jambo lililo sawa kulingana na viwango vya Mungu vya mema na mabaya.—Mwa 15:6; Kum 6:25; Met 11:4; Sef 2:3; Mt 6:33.

Uajemi; Waajemi. Nchi na watu wanaotajwa mara nyingi pamoja na Wamedji, ni wazi kwamba wana uhusiano nao. Katika historia yao ya mapema, Waajemi walimiliki tu eneo lililo upande wa kusini magharibi wa uwanda wa Irani. Chini ya Koreshi Mkuu (ambaye kulingana na wanahistoria fulani wa kale alizaliwa na baba Mwajemi na mama Mmedi), Waajemi walikuwa na mamlaka kuliko Wamedji, ingawa milki hiyo iliendelea kuwa na falme mbili. Koreshi aliishinda Milki ya Babiloni katika mwaka wa 539 K.W.K. naye akawaruhusu Wayahudi walio-kuwa utekwani warudi katika nchi yao. Milki ya Uajemi ilianza kwenye Mto Indus upande wa mashariki mpaka kwenye Bahari ya Aegea upande wa magharibi. Wayahudi walikuwa chini ya utawala wa Waajemi mpaka Aleksanda Mkuu alipowashinda Waajemi katika mwaka wa 331 K.W.K. Danieli aliona mapema Milki ya Uajemi katika maono, nayo inatajwa pia katika vitabu vya Biblia kama vile Ezra, Nehemia, na Esta. (Ezr 1:1; Da 5:28)—Angalia Nyongeza B9.

Uasherati. Neno hili linatokana na neno la Kigiriki *porneia*, ambalo ni neno linalotumiwa katika Maandiko kurejelea baadhi ya vitendo vya ngono ambavyo Mungu anakataza. Linatia ndani uzini, ukahaba, ngono kati ya watu ambao hawajafunga ndoa, ngono kati ya watu wa jinsia moja, na kufanya ngono na wanyama. Linatumia kwa njia ya mfano katika kitabu cha Ufunuo kueleza jinsi kahaba wa kidini anayeitwa “Babiloni Mkubwa” anavyoshirikiana na watawala wa ulimwengu huu kupata mamlaka na utajiri. (Ufu 14:8; 17:2; 18:3; Mt 5:32; Mdo 15:29; Gal 5:19)—Tazama KAHABA.

Uasi imani. Katika Kigiriki neno hili (*a-po-sta-si'a*) linatokana na kitenzi ambacho kihalisi kinamaanisha “kusimama mbali na.” Nomino hiyo inamaanisha “kuondoka, kuacha, au kuasi.” Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, neno “uasi imani” hutumiwa hasa kuwarejelea wale ambao wameasi ibada ya kweli.—Met 11:9; Mdo 21:21; 2Th 2:3.

Ubani. Utomvu uliokaushwa wa miti na vichaka vya jamii fulani ya mimea inayoitwa *Boswellia*. Ubani huo ulipochomwa, ulitoa harufu nzuri sana. Ulikuwa mojawapo ya viungo vya uvumba mtakatifu uliotumiwa katika hema la ibada na hekaluni. Ulitolewa pia pamoja na matoleo ya nafaka, nao uliwekwa juu ya kila safu ya mikate ya wonyesho ndani ya Patakatifu.—Kut 30:34-36; Law 2:1; 24:7; Mt 2:11.

Ubatizo; Batiza. Kitenzi “batiza” kinamaanisha “zamisha,” au tumbukiza ndani ya maji. Yesu alifanya ubatizo uwe takwa kwa wafuasi wake. Maandiko yanataja pia ubatizo uliofanywa na Yohana, kubatizwa kwa roho takatifu, kubatizwa kwa moto, na ubatizo mwingineo.—Mt 3:11, 16; 28:19; Yoh 3:23; 1Pe 3:21.

Ufalme wa Mungu. Maneno hayo yanatumiwa hasa kumaanisha enzi kuu ya Mungu inayowakilisha na serikali ya kifalme ya Mwana wake, Kristo Yesu.—Mt 12:28; Lu 4:43; 1Ko 15:50.

Ufilisti; Wafilisti. Nchi iliyo kwenye pwani ya kusini ya Israeli ambayo baadaye iliitwa Ufilisti. Wahamiaji kutoka Krete ambao waliishi katika nchi hiyo waliitwa Wafilisti. Daudi aliwashinda, lakini waliendelea kuwa huru na daima walikuwa maadui wa Israeli. (Kut 13:17; 1Sa 17:4; Am 9:7)—Angalia Nyongeza B4.

Ufufuo. Kuinuka kutoka katika kifo. Neno la Kigiriki *a-na'sta-sis* kihalisi linamaanisha “kuinuka; kusimama.” Biblia ina masimulizi tisa ya ufufuo, kutia ndani simulizi kuhusu Yehova Mungu aki-mfufua Yesu. Ingawa Eliya, Elisha, Yesu, Petro, na Paulo waliwafufua watu, ni wazi kwamba walifanya miujiza hiyo kwa nguvu za Mungu. Ufufuo wa “waadilifu na wasio waadilifu pia” utakaofanyika duniani ni muhimu katika kutimiza kusudi la Mungu. (Mdo 24:15) Biblia inataja pia ufufuo wa kwenda mbinguni, unaoitwa ufufuo “wa mapema” au “wa kwanza,” ambao ni ufufuo wa ndugu za Yesu walioitiwa mafuta kwa roho.—Flp 3:11; Ufu 20:5, 6; Yoh 5:28, 29; 11:25.

Ujitoaji-kimungu. Heshima, ibada, na utumishi unaoitolewa kwa Yehova Mungu, na ushikamani-fu kwa enzi yake kuu ya ulimwengu mzima.—1Ti 4:8; 2Ti 3:12.

Ukaldayo; Wakaldayo. Awali maneno hayo yalirejelea nchi na watu walioishi katika eneo la mlangano bahari wa Mto Tigri na Mto Efrati; baada ya

muda maneno hayo yalitumiwa kurejelea eneo lote la Babilonia na watu wake. Neno “Wakaldayo” lilitumiwa pia kuwahuu watu fulani wasomi waliojifunza sayansi, historia, lugha, na elimu ya nyota lakini ambao walizoea pia kufanya uchawi na unajimu.—Ezr 5:12; Da 4:7; Mdo 7:4.

Ukoma; Mwenye ukoma. Ugonjwa mbaya sana wa ngozi. Ukoma unaoitajwa katika Maandiko haulingani sana na ugonjwa unaoitwa ukoma leo, kwa maana zamani ugonjwa huo uli-waathiri wanadamu na pia mavazi na nyumba. Mtu mwenye ugonjwa huo anaitwa mtu mwenye ukoma.—Law 14:54, 55; Lu 5:12.

Ulozi. Matumizi ya nguvu zinazojulikana kwamba zinatoka kwa roho waovu.—2Ny 33:6.

Umalizio wa mfumo wa mambo. Kipindi cha wakati kinachotangulia mwisho wa mfumo wa mambo, au hali ya mambo, kipindi ambacho kinangozwa na Shetani. Kinaenda sambamba na kuwapo kwa Kristo. Chini ya mwongozo wa Yesu, malaika watawatenganisha waovu kutoka kwa waadilifu na kuwaangamiza. (Mt 13:40-42, 49) Wanafunzi wa Yesu walitaka kujua wakati ambapo “umalizio” huo ungekuja. (Mt 24:3) Kabla ya kurudi mbinguni, Yesu aliwaahidi wafuasi wake kwamba angekuwa pamoja nao mpaka wakati huo.—Mt 28:20.

Unabii. Ujumbe ulioongozwa na roho takatifu, iwe ni unfunuo kuhusu mapenzi ya Mungu au tangazo la mapenzi yake. Unabii unaweza kuwa fundisho la maadili lililoongozwa na roho takatifu, amri ya Mungu au hukumu, au tangazo la jambo litakalotokea.—Eze 37:9, 10; Da 9:24; Mt 13:14; 2Pe 1:20, 21.

Upatanisho.—Tazama KUFUNIKA DHAMBI.

Upendo mshikamanifu. Kwa kawaida usemi huo unatafsiriwa kutokana na neno la Kiebrania *che'sedh*, linaloanisha upendo unaochochea na uwajibikaji au ujitoaji, utimilifu, ushikamanifu, na kufungamana kwa dhiti. Mara nyingi usemi huo unatumiwa kurejelea upendo wa Mungu kwa wanadamu, lakini pia wanadamu wanaweza kuwa na upendo huo kati yao.—Kut 34:6; Ru 3:10.

Urimu na Thumimu. Ni vitu vilivyotumiwa na kuhani mkuu kama kura ili kujua mapenzi ya Mungu maswali muhimu ya kitaifa yalipohitaji majibu kutoka kwa Yehova. Urimu na Thumimu viliwekwa ndani ya kifuko cha kifua cha kuhani mkuu alipoingia katika hema la ibada. Inaonekana kwamba vitu hivyo havikutumiwa tena Wababiloni walipoharibu Yerusalemu.—Kut 28:30; Ne 7:65.

Ushahidi. Kwa kawaida “Ushahidi” ni zile Amri Kumi zilizoandikwa kwenye mabamba mawili ya mawe ambayo Musa alipewa.—Kut 31:18.

Ushuru. Malipo ambayo Taifa au mtawala alimpa mwingine ikiwa ishara ya ujitiisho, ili kudumisha amani au kupata ulinzi. (2Fa 3:4; 18:14-16; 2Nya 17:11) Neno hilo pia linatumia kumaanisha kodi ambayo mtu mmoja alitowza. —Ne 5:4; Ro 13:7.

Utangulizi. Maneno yanayopatikana mwanzoni mwa zaburi ambayo yanamtambuliha mabandishi, yanaeleza habari za ziada kuhusu zaburi hiyo, yanatoa maagizo ya kimuziki, au yanaonyesha wakati zaburi hiyo iliipombwa au kusudi lake.—Angalia utangulizi wa Zaburi 3, 4, 5, 6, 7, 30, 38, 60, 92, 102.

Utete wa kupimia. Utete wa kupimia ulikuwa na urefu wa mikono sita. Kulingana na kipimo cha kawaida cha mkono, utete huo ulikuwa na urefu wa mita 2.67 (futi 8.75); kulingana na kipimo cha mkono mrefu, ulikuwa na urefu wa mita 3.11 (futi 10.2). (Eze 40:3, 5; Ufu 11:1)—Angalia Nyongeza B14.

Utete. Neno linalotumiwa kurejelea mimea mingi ambayo kwa kawaida inakuwa katika sehemu zenye umajimaji. Mmaa unaoitwa utete katika Maandiko mengi ni *Arundo donax*. (Ayu 8:11; Isa 42:3; Mt 27:29; Ufu 11:1)—Tazama UTETE WA KUPIMIA.

Utumishi mtakatifu. Huduma, au kazi, iliyo takatifu, ambayo inahusiana moja kwa moja na ibada ambayo mtu anamtotea Mungu.—Ro 12:1; Ufu 7:15.

Uvumba. Mchanganyiko wa utomvu wa aina mbalimbali wenye harufu nzuri na zeri unaoungua polepole na kutokeza harufu yenye manukato. Uvumba wa pekee wenye viungo vinne ulitengenezwa ili utumiwe katika hema la ibada na hekaluni. Ulifukizwa asubuhi na usiku kwenye madhabahu ya uvumba ndani ya Patakatifu, na katika Siku ya Kufunika Dhambi, ulifukizwa ndani ya Patakatifu Zaidi. Ulifananiha sala zinazokubalika za watumishi waaminifu wa Mungu. Wakristo hawakuwa chini ya takwa la kutumia uvumba.—Kut 30:34, 35; Law 16:13; Ufu 5:8.

Uzinz. Ni ngono inayofanywa kwa hiari kati ya mwanamume aliyeoa na mwanamke ambaye si mke wake au kati ya mwanamke aliyeolewa na mwanamume ambaye si mume wake.—Kut 20:14; Mt 5:27; 19:9.

V

Vyetezo. Vifaa vilivyotengenezwa kwa dhahabu, fedha, au shaba, ambavyo vilitumiwa katika hema la ibada na hekalu kufukizwa uvumba na kuondolea makaa ya mawe kwenye madhabahu ya dhambi na tamba zilizoungua za taa kutoka katika vinara vya taa vya dhahabu.—Kut 37:23; 2Nya 26:19; Ebr 9:4.

W

Waamuzi. Wanaume waliowekwa na Yehova ili kuwaokoa watu wake kabla ya kipindi cha wanadamu waliotawala wakiwa wafalme wa Israeli. —Amu 2:16.

Wafuasi wa chama cha Herode.—Tazama HERO-DE; WAFUASI WA CHAMA CHA.

Wakfu, ishara takatifu ya. Bamba linalong'aa la dhahabu safi lililochochwa maneno haya ya Kiebrania, "Utakatifu ni wa Yehova." Liliwekwa upande wa mbebe wa kilemba cha kuhani mkuu. (Kut 39:30)—Angalia Nyongeza B5.

Wakili Mkuu. Katika Kigiriki, kimsingi neno hili linamaanisha "Kiongozi Mkuu." Linaonyesha jukumu muhimu la Yesu Kristo la kuaweka huru wanadamu waaminifu kutoka katika madhara yanayoangamiza ya dhambi na kuwaongoza kwenye uzima wa milele.—Mdo 3:15; 5:31; Ebr 2:10; 12:2.

Walenzi wa Mfalme. Kikundi cha wanajeshi Waroma kilichoanzishwa ili kumlinda maliki wa Roma. Kikundi hicho kilikuja kuwa na ushawishi mkubwa sana wa kisiasa katika kumuunga mkono au kumwondoa maliki.—Flp 1:13.

Wamedi; Umedi. Wazao wa Madai, mwana wa Yafethi; waliishi katika eneo lenye milima la uwanda wa Irani ambalo lilikuja kuwa nchi ya Umedi. Wamedi walijiunga na Wababiloni ili kuwashinda Waashuru. Wakati huo, nchi ya Uajemi ilikuwa mkoa wa Umedi, lakini Koreshi aliani na nchi ya Umedi ikaungana na Uajemi zikatokeza Milki ya Umedi na Uajemi ambayo ilishinda Milki mpya ya Babiloni katika mwaka wa 539 K.W.K. Wamedi walikuwa Yerusalemu katika siku ya Pentekoste ya mwaka wa 33 W.K. (Da 5:28, 31; Mdo 2:9)—Angalia Nyongeza B9.

Wana wa Haruni. Wazao wa Haruni, mjuukuu wa Lawi; Haruni alichaguliwa kuwa kuhani mkuu wa kwanza chini wa Sheria ya Musa. Wana wa Haruni walitekeleza majukumu ya kuhani katika hema la ibada na hekaluni.—1Nya 23:28.

Wanafalsafa Waepikurea. Wafuasi wa wanafalsafa Mgiriki aliyeitwa Epicurus (341-270 K.W.K.). Falsafa yao ilitegemea wazo la kwamba lengo kuu maishani mwa mtu ni kupata raha.—Mdo 17:18.

Wanafalsafa Wastoa. Jamii ya wanafalsafa Wagiriki walioamini kwamba furaha inahusisha kuishi kulingana na mambo ya asili na kutumia akili. Kulingana na maoni yao, mtu aliyekwa na hekima ya kweli, alipuuzwa maumivu na furaha.—Mdo 17:18.

Wanefili. Wana wakatili waliozaliwa baada ya malaika waliojivika miili ya kibinadamu kufanya ngono na mabinti wa wanadamu kabla ya Ghairika.—Mwa 6:4.

Wanethini. Watumishi au wahudumu wa hekaluni ambao hawakuwa Waisraeli. Kihalisi neno la Kiebrania linamaanisha "Waliotolewa," kuonyesha kwamba walikuwa wametolewa kwa ajili ya utumishi wa hekaluni. Inaelekea kwamba Wanethini wengi walikuwa wazao wa Wagibeoni, ambao Yohua alikuwa amewafanya kuwa "wakusanyaji wa kuni na watekaji wa maji kwa ajili ya Waisraeli na kwa ajili ya madhabahu ya Yehova."—Yos 9:23, 27; 1Nya 9:2; Ezr 8:17.

Wasamaria. Mwanzoni neno hili lilirejelea Waisraeli wa ufalme wa kaskazini wa makabila kumi, lakini baada ya nchi ya Samaria kushindwa na Waashuru katika mwaka wa 740 K.W.K., neno hilo lilitia ndani wageni walioletwa na Waashuru. Katika siku za Yesu, neno hilo halikuhusianishwa na jamii fulani au siasa, badala yake, kwa kawaida lilimaanisha wafuasi wa madhehebu ya kidini ambayo yalikuwa karibu na jiji la kale la Shekemu na Samaria. Wafuasi wa madhehebu hayo walifuata mafundisho fulani yaliyokuwa tofauti sana na ya dini ya Kiyahudi.—Yoh 8:48.

Wimbo wa maombolezo. Wimbo wa maneno au wa ala, wenye hisia za huzuni kubwa, kama huzuni inayoonyeshwa na mtu aliyefiwa na rafiki yake au na mpendwa wake; wimbo wa majonzi.—2Sa 1:17; Zb 7:Utangulizi.

Wimbo wa Safari za Kupanda. Maneno ya utangulizi ya Zaburi 120-134. Ingawa watu wana maoni mbalimbali kuhusu maana ya maneno hayo, wengi wanaamini kwamba zaburi hizo 15 ziliimbwa na waabudu Waisraeli wenye shangwe walipokuwa 'wakipanda' kwenenda Yerusalemu, jiji lililokuwa juu katika milima ya Yuda, ili kuhudhuria sherehe tatu kuu za kila mwaka.

Y

Yakobo. Mwana wa Isaka na Rebeka. Baadaye Mungu alimpa jina Israeli, naye akawa mzee wa ukoo wa watu wa Israeli (ambao pia waliitwa Waisraeli na baadaye, Wayahudi). Alikuwa baba ya wana 12 ambao, pamoja na wazao wao, walifanyiza makabila 12 ya taifa la Israeli. Jina Yakobo lililendelea kutumiwa kurejelea taifa la Israeli au watu wa Israeli.—Mwa 32:28; Mt 22:32.

Yeduthuni. Maana ya neno hili linalopatikana katika utangulizi wa Zaburi 39, 62, na 77 haijulikani vizuri. Inaonekana kwamba utangulizi huo ni maagizo ya kuimba zaburi hizo, labda yanatambulisha mtindo au ala ya muziki. Kulikuwa na mwanamuziki Mlawi aliyelitwa Yeduthuni, kwa hiyo huenda mtindo wa Yeduthuni au ala ya kuimba kwa mtindo huo ilihusianishwa naye au wanawe.

Yehova. Kwa kawaida jina hili ni tafsiri ya Kiswahili ya Tetragramaton (zile herufi nne za Kiebra-

nia za jina la kibinafsi la Mungu), nalo linapatikana zaidi ya mara 7,000 katika tafsiri hii.—Angalia Nyongeza A4 na A5.

Yuda. Mwana wa nne wa Yakobo aliyezaliwa na mke wake Lea. Katika unabii aliotoa alipokuwa akikaribia kufa, Yakobo alitabiri kwamba mtawala mkuu wa wa kudumu angetoka katika ukoo wa Yuda. Akiwa mwanadamu, Yesu alitoka Yuda. Pia, jina Yuda linarejelea kabila hilo na baadaye lilirejelea ufalme ulioitwa kwa jina hilo. Ufalme wa Yuda unatajwa pia kuwa ufalme wa kusini, na ulifanyizwa na makabila haya ya Israeli, yaani, kabila la Yuda na la Benjamini, na pia makuhani na Walawi. Kabila la Yuda liliishi upande wa kusini wa nchi iliyotia ndani Yerusalemu na hekalu.—Mwa 29:35; 49:10; 1Fa 4:20; Ebr 7:14.

Z

Zaburi. Wimbo wa kumsifu Mungu. Zaburi zilitungwa kama muziki na kuimba na waabudu, kama wakati ambapo watu walimwabudu Yehova Mungu katika hekalu lake kule Yerusalemu.—Lu 20:42; Mdo 13:33; Yak 5:13.

Zawadi za rehema. Zawadi zilizotolewa ili kumsaidia mtu mwenye uhitaji. Zawadi hizo hazitajwi moja kwa moja katika Maandiko ya Kiebrania, lakini Sheria iliwapu Waisraeli maagizo husuka kuhusu wajibu wao wa kuwasaidia maskini.—Mt 6:2.

Ze. Mungu mkuu wa Wagiriki walioabudu miungu mingi. Kule Litra, Barnaba alitwa kima-kosa Zeu. Maandishi ya kale yaliyochoyongwa yaliyopatikana karibu na Litra yanataja "makuhani wa Zeu" na "mungu-jua Zeu." Meli alimosafiria Paulo kutoka katika kisiwa cha Malta ilikuwa na sanamu ya "Wana wa Zeu," juu upande wa mbele, yaani, ndugu mapacha Castor na Pollux.—Mdo 14:12; 28:11.

Zivu. Jina la awali la mwezi wa pili katika kalenda takatifu ya Wayahudi na jina la mwezi wa nane katika kalenda iliyotumiwa na watu wote. Mwezi huo ulianzia katikati ya mwezi wa Aprili mpaka katikati ya mwezi wa Mei. Unaitwa Iyari katika Talmudi ya Wayahudi na pia katika maandishi mengine baada ya Wayahudi kutoka uhamishoni Babiloni. (1Fa 6:37)—Angalia Nyongeza B15.

Ziwa la moto. Mahali pa mfano 'panapowaka moto na kiberiti,' panafanuliwa pia kuwa "kifo cha pili." Watenda dhambi wasiotubu, Ibilisi, na hata kifo na Kaburi (au, Hadesi) vinatupwa humo. Kwa kuwa kiumbe wa roho na pia kifo na Hadesi, vitu ambavyo haviwezi kuathiriwa na moto, vinatajwa kuwa vinatupwa humo, hilo linaonyesha kwamba ziwa hili ni mfano, si mfano wa mateso ya milele, bali ni mfano wa maangamizi ya milele.—Ufu 19:20; 20:14, 15; 21:8.

Nyongeza A

Kanuni za Kutafsiri Biblia	A1
Sehemu za Toleo Hili	A2
Jinsi Biblia Ilivyotufikia	A3
Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kiebrania	A4
Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo	A5
Chati: Manabii na Wafalme wa Yuda na Israeli	A6
Matukio Muhimu Katika Maisha ya Yesu Duniani	A7

Mwanzoni Biblia iliandikwa katika Kiebrania, Kiaramu, na Kigiriki cha kale. Leo inapatikana ikiwa nzi-ma au kwa sehemu katika lugha 3,000 hivi. Idadi kubwa ya watu wanaosoma Biblia hawaelewi lugha za awali na hivyo lazima wategemee tafsiri. Ni kanuni gani zinapaswa kufuatwa katika kutafsiri Biblia, na zilitumiwaje katika kutafsiri *Biblia Takatifu* –*Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*?

Huenda wengine wakafikiri kwamba tafsiri ya neno kwa neno inaweza kuwasaidia wasomaji wapate maana inayokaribiana zaidi na ile iliyo katika lugha za awali. Hata hivyo, si lazima iwe hivyo. Fikiria baadhi ya sababu:

- Hakuna lugha mbili zinazofanana kabisa katika sarufi, msamiati, na muundo wa sentensi. Profesa wa Kiebrania, S. R. Driver, aliandika kwamba lugha “hazitofautiani tu katika sarufi na mizizi, bali pia . . . jinsi ambavyo mawazo yanaunganishwa katika sentensi.” Lugha tofauti hutumia njia tofauti za kufikiri. “Kwa hiyo,” anaendelea kusema Profesa Driver, “miundo ya sentensi katika lugha mbalimbali hutofautiana.”
- Hakuna lugha yoyote ya kisasa inayofanana kabisa na msamiati na sarufi ya Kiebrania, Kiaramu, na Kigiriki kilichotumiwa kuandika Biblia, kwa hiyo, huenda tafsiri ya neno kwa neno ya Biblia isieleweke au hata nyakati nyingine ikapotosha maana.
- Maana ya neno au maneno inaweza kubadilika ikitegemea muktadha.

Katika baadhi ya sehemu, mtafsiri anaweza kutafsiri lugha ya awali neno na kwa neno kwa usahihi, lakini anapaswa kuwa makini sana.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano inayoonyesha jinsi tafsiri ya neno kwa neno inavyoweza kueleweka vibaya:

- Maandiko hutumia maneno ‘kulala usingizi’ kumaa-nisha usingizi halisi na usingizi wa kifo. (Mathayo 28:13; Matendo 7:60) Maneno hayo yanapotumiwa kwenye muktadha

unaorejezea kifo, watafsiri wa Biblia wanaweza kutumia maneno kama ‘kulala usingizi katika kifo,’ ambayo humsaidia msojaji wa kisasa aelewe maana.—1 Wakorintho 7:39; 1 Wathesalonike 4:13; 2 Petro 3:4.

- Mtume Paulo alitumia maneno yanayopatikana katika Waefeso 4:14 ambayo yanaweza kutafsiriwa neno kwa neno kuwa “katika mchezo wa dadu wa wanaume.” Msemu huo wa kale unarejezea zoea la kuwadanganya watu kwa kutumia dadu. Katika lugha nyingi, tafsiri ya neno kwa neno ya msemu huo haieleweki vizuri. Kutafsiri msemu huo kuwa “udanganyifu wa watu” ni njia iliyo wazi zaidi ya kutokeza maana.
- Andiko la Waroma 12:11 linatumia msemu wa Kigiriki ambao ukitafsiriwa neno na kwa neno unamaanisha “katika kuchemka kwa roho.” Katika Kiswahili, maneno hayo hayatokezi maana iliyokusudiwa, kwa hiyo katika tafsiri hii yametafsiriwa kuwa ‘kukwaka roho.’
- Katika mahubiri yake maarufu ya mlimani, Yesu alitumia maneno ambayo mara nyingi hutafsiriwa kuwa “Heri walio maskini wa roho.” (Mathayo 5:3, *Union Version*) Lakini katika lugha nyingi, tafsiri ya neno kwa neno ya mstari huo haieleweki. Katika visa fulani, tafsiri ya neno kwa neno inaweza

kumaanisha kwamba “maskini wa roho” ni watu walio na matatizo ya kiakili au walio dhaifu na wasio na msimamo. Hata hivyo, hapa Yesu alikuwa akiwafundisha watu kwamba furaha yao haikutegemea kutosheleza mahitaji yao ya kimwili, bali kutambua kwamba wanahitaji mwongozo wa Mungu. (Luka 6:20) Kwa hiyo, maneno kama vile “wale wanaotambua uhitaji wao wa kiroho” au “wale wanaotambua kwamba wanahitaji Mungu” hutokeza kwa usahihi maana ya maneno ya awali.—Mathayo 5:3; *The New Testament in Modern English*.

- Katika muktadha mbalimbali, neno la Kiebrania linalotafsiriwa kuwa “wivu” linalingana na maana ya neno la Kiswahili, yaani, kukasirika kwa sababu rafiki wa karibu amekosa uaminifu au kuwaonea wivu watu kwa sababu ya mali zao. (Methali 6:34; Isaya 11:13) Hata hivyo, neno hilo la Kiebrania lina maana nzuri. Kwa mfano, linaweza kutumiwa kumaanisha “bidii,” au ulinzi ambao Yehova anawapa watumishi wake au jinsi

ΟΙΠΤΩΧΟΙ
ΤΩΠΝΕΥΜΑΤΙ

MATHAYO 5:3

Tafsiri ya neno
kwa neno: “maskini
wa roho”

Wazo: “wale
wanaotambua
uhitaji wao wa
kiroho”

anavyotaka ‘wamwabudu yeye peke yake.’ (Kutoka 34:14; 2 Wafalme 19:31; Ezekieli 5:13; Zekaria 8:2) Pia linaweza kutumiwa kumaanisha “bidii” ya watumishi wake waaminifu kwa ajili ya Mungu na ibada yake au jinsi ambavyo ‘hawavumilii ushinda-ni wowote’ kumwelekea.—Zaburi 69:9; 119:139; Hesabu 25:11.

- Neno la Kiebrania ambalo mara nyingi hurejelea mkono wa mwanadamu lina maana mbalimbali. Ikitegemea muktadha neno hilo linaweza kutafsiriwa kuwa “mamlaka,” “ukarimu,” au “nguvu.” (2 Samweli 8:3; 1 Wafalme 10:13; Methali 18:21) Kwa kweli, neno hilo limetafsiriwa kwa zaidi ya njia 40 tofauti-tofauti katika toleo la Kiingereza la *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

י

Neno la Kiebrania
yadh kwa kawaida
hutafsiriwa kuwa
“mkono,” lakini
ikitegemea muktadha,
neno hili linaweza
kutafsiriwa kuwa
“mamlaka,” “ukarimu,”
“nguvu,” na kwa njia
nyingine nyingi

Kutokana na sababu hizo, kutafsiri Biblia kunahusisha mengi zaidi ya kutafsiri neno la lugha ya awali kwa kutumia neno lilelile kila mara. Mtafsiri anapaswa kutumia busara ili kuchagua maneno ambayo yanawakilisha vizuri mawazo ya maandishi ya lugha ya awali. Isitoshe, anapaswa kupanga sentensi katika njia inayofuata sheria za sarufi za lugha inayolengwa, na hivyo kufanya maandishi yasomeke kwa urahisi.

Wakati huohuo mtafsiri hapaswi kupita mipaka anapotumia maneno tofauti ili kueleza maandishi. Mtafsiri ambaye bila kujali anafanua ujumbe wa Biblia kulingana na jinsi anavyoelewa wazo kuu anaweza kupotosha maana ya maandishi. Jinsi gani? Mtafsiri anaweza kuingiza kimakosa maoni

yake kuhusu maana ya maandishi ya awali au huenda akaondoa habari muhimu zilizo kwenye maandishi ya awali. Kwa hiyo, ingawa huenda tafsiri za Biblia zilizofafanuliwa zikasomeka kwa urahisi, nyakati nyingine huenda uhuru huo ukafanya wasomaji wasipate ujumbe halisi wa maandishi.

Ni rahisi kwa mtafsiri kuathiriwa na msimamo wa kidini. Kwa mfanano, andiko la Mathayo 7:13 linasema “Barabara inayoongoza kwenye uharibifu ina nafasi kubwa.” Baadhi ya watafsiri ambao labda wameathiriwa na msimamo wa kidini, wametumia maneno “moto wa mateso” badala ya maana halisi ya neno la Kigiriki, yaani, “uharibifu.”

Pia, mtafsiri anapaswa kukumbuka kwamba Biblia iliandikwa kwa kutumia lugha iliyotumiwa na watu wa kawaida, kama vile waku-
lima, wachungaji, na wavuvi. (Nehemia 8:8, 12; Matendo 4:13)

Kwa hiyo, tafsiri nzuri ya Biblia hufanya ujumbe wake ueleweke kwa watu wanyoofu, wa malezi mbalimbali. Maneno yaliyo wazi, ya kawaida, na yanayoeleweka kwa urahisi yanafaa kuliko maneno ambayo hayatumwi sana na watu wa kawaida.

Idadi kubwa ya watafsiri wa Biblia wamefanya uamuzi usio na misingi wa kuondoa jina la Mungu, Yehova, kutoka katika tafsiri za kisasa ingawa jina hilo linapatikana katika hati za kale za Biblia. (Angalia Nyongeza A4.) Tafsiri nyingi huondoa jina hilo na kutumia jina la cheo, kama vile “Bwana,” na nyingine hata huficha ukweli wa kwamba Mungu ana jina. Kwa mfano, katika baadhi ya tafsiri, sala ya Yesu kwenye Yohana 17:26 inasema: “Nimekufanya ujulikane kwao,” na kwenye Yohana 17:6, “Nimekufunua kwa wale ulionipa.” Hata hivyo, tafsiri sahihi ya sala ya Yesu inasema: “Nimewajulisha *jina lako*,” na “Nimelifunua *jina lako* kwa watu ulionipa.”

Kama ilivyotajwa katika utangulizi wa toleo la kwanza la Kiingereza la *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*: “Hatufafanui Maandiko. Tumejitahidi kutafsiri neno kwa neno inapowezekana, mahali ambapo misemo ya Kiingereza ya kisasa inaruhusu na mahali ambapo tafsiri ya neno kwa neno haifichi maana.” Kwa hiyo, Halmashauri ya Biblia ya Tafsiri ya Ulimwengu Mpya imejitahidi kusawazisha kati ya kutumia maneno na misemo inayofanana na ile iliyo kwenye hati za kale, na wakati huohuo, kuepuka maneno ambayo hayaeleweki au yanayoficha mawazo yaliyokusudiwa. Matokeo ni kwamba Biblia inaweza kusomeka kwa urahisi na msomaji anaweza kuwa na uhakika kabisa kwamba ujumbe wa Biblia ulioongozwa na roho ya Mungu umetafsiriwa kwa usahihi.—1 Wathesalonike 2:13.

Tafsiri inayotegemeka inapaswa:

- Kulitakasa jina la Mungu kwa kulirudisha mahali pake pana-pofaa katika Maandiko.—Mathayo 6:9.
- Kuwasilisha kwa usahihi ujumbe wa awali ulioongozwa na roho ya Mungu.—2 Timotheo 3:16.
- Kutafsiri neno kwa neno ikiwa maneno na muundo wa lugha inayolengwa unaruhusu kutafsiri maandishi ya awali kwa njia hiyo.
- Kuwasilisha kwa usahihi maana ya neno au maneno ikiwa tafsiri ya neno kwa neno inaweza kupotosha au kuficha maana.
- Kutumia lugha ya kawaida, inayoeleweka kwa urahisi na iliyo rahisi kusoma.—Nehemia 8:8, 12.

Tafsiri ya Ulimwengu Mpya ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo ilitolewa katika Kiingereza mwaka wa 1950, na toleo zima la *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* lilichapishwa mwaka wa 1961. Tangu wakati huo makumi ya mamilioni ya wasomaji katika lugha zaidi ya 180 wamefaidika na tafsiri hii sahihi na inayosomeka ya Maandiko Matakatifu iliyotafsiriwa kutoka kwa lugha za awali.

Halmashauri ya sasa ya Biblia ya Tafsiri ya Ulimwengu Mpya inatambua uhitaji wa kutumia lugha inayogusa mioyo ya wasomaji wa kisasa. Kwa sababu hiyo, kanuni kadhaa za muundo na msamiati zilifuatwa katika tafsiri hii ili kutimiza mambo yafuatayo:

- **Kutumia lugha ya kisasa na inayoeleweka.** Kwa mfano, neno “ustahimilivu” linaweza kueleweka kimakosa kumaanisha “mtu anayeteseka kwa muda mrefu.” Hata hivyo, wazo linalokusudiwa ni kujizua kwa hiari, ambalo linatokezwa vizuri zaidi kwa kutumia neno “subira.” (Wagalatia 5:22) Katika toleo hili, maneno “karamu za kupindukia” yametafsiriwa kuwa “karamu zenye vurugu.” (Wagalatia 5:19-21) Maneno “wakati usio na kipimo” yaliondolewa na badala yake maneno kama vile “milele,” “kudumu,” “zamani za kale” yakatumiwa ili kutokeza maana iliyokusudiwa katika kila muktadha.—Mwanzo 3:22; Kutoka 31:16; Zaburi 90:2; Mhubiri 1:4; Mika 5:2.

Katika Kiebrania na Kigiriki cha kale neno “mbegu” linaweza kumaanisha mbegu ya mmea na pia uzao wa wanadamu, au wazao, au shahawa. Kwa kuwa si kawaida katika lugha ya Kiswahili kutumia neno “mbegu” kurejelea wanadamu, neno hilo liliondolewa na badala yake maneno yanayotokeza maana inayokusudiwa yakatumiwa kulingana na muktadha. (Mwanzo 1:11; 22:17; 48:4; Mathayo 22:24; Yohana 8:37) Mara nyingi, neno “uzao” sasa linatumiwa kurejelea ahadi iliyotolewa katika Edeni, kwenye Mwanzo 3:15.

- **Maneno yaliyo katika Biblia yafafanuliwa.** Katika matoleo yaliyotangulia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* ya Kiingereza, neno la Kiebrania *ne’phesh* na neno la Kigiriki *psy-khe’* kila mara yalitafsiriwa kuwa “nafsi.” Kwa sababu ya maoni mengi

yasiyo ya kweli kuhusu maana ya neno “nafsi,” mbinu hiyo ilimsaidia msomaji kuelewa jinsi waandikaji wa Biblia walioongozwa na roho ya Mungu walivyotumia maneno hayo ya lugha ya awali. Ikitegemea muktadha, maneno hayo yanaweza kumaanisha (1) mtu, (2) uhai wa mwanadamu, (3) viumbe walio hai, (4) tamaa na hamu ya mtu au, mara nyingine, (5) hata watu waliokufa. Hata hivyo, kwa kuwa matumizi kama hayo ya neno “nafsi” si ya kawaida katika Kiswahili, uamuzi ulifanywa ili kutafsiri maneno hayo ya lugha ya awali kulingana na maana iliyokusudiwa, mara nyingi yakiwa na maelezo ya chini yanayosema “Au ‘nafsi.’” (Kwa mfano, angalia, Mwanzo 1:20; 2:7; Mambo ya Walawi 19:28; Zaburi 3:2; Methali 16:26; Mathayo 6:25.) Hata hivyo, katika mashairi na mistari inayojulikana, neno “nafsi” limedumishwa, pamoja na maelezo ya chini yanayoelekeza kwenye Kamusi au yanayoonyesha maana nyingine.—Kumbukumbu la Torati 6:5; Zaburi 131:2; Methali 2:10; Mathayo 22:37.

Vivyo hivyo, neno figo lilidumishwa linaporejelea kiungo halisi. Hata hivyo, linapotumiwa kwa njia ya mfano kama vile kwenye Zaburi 7:9 na 26:2 na Ufunuo 2:23, wazo lililokusudiwa la “hisia za ndani kabisa” au “mawazo ya ndani kabisa” limeandikwa kwenye mistari, na tafsiri ya neno kwa neno kwenye maelezo ya chini.

Kama ilivyo katika Kiebrania na Kigiriki, neno la Kiswahili “moyo” lina maana halisi na maana ya mfano, basi mara nyingi lilidumishwa katika mistari. Hata hivyo, katika sehemu chache ambapo maana haikueleweka, ujumbe ulitafsiriwa kwa njia iliyo wazi zaidi. Kwa mfano, katika kitabu cha Methali, maneno “aliyepungukiwa moyoni” sasa yametafsiriwa kuwa “asiye na busara,” nayo tafsiri ya neno kwa neno imewekwa kwenye maelezo ya chini. (Methali 6:32; 7:7) Maneno mengine, kama vile, “unono,” “mwili,” na “pembe,” yalishughulikiwa kwa njia hiyo, kulingana na muktadha. (Mwanzo 45:18; Mhubiri 5:6; Ayubu 16:15) Baadhi ya maneno hayo yanafanuliwa katika “Kamusi ya Maneno ya Biblia.”

- **Kusomeka kwa urahisi.** Katika matoleo yaliyotangulia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*, vitenzi visaidizi vilitumiwa kuonyesha ikiwa kitenzi cha Kiebrania kilikuwa kimekamiliika au la. Kwa mfano, kitendo kinachoendelea ambacho mara nyingi huelezwa kwa kutumia kitenzi ambacho hakijakamiliika, kilionyeshwa kwa kutumia maneno kama “akaendelea,” “ikawa,” na kadhalika. Mkazo ambao mara nyingi huwasilishwa na kitenzi cha Kiebrania kilichokamiliika ulionyeshwa

kwa kuongezea maneno “kwa hakika,” “lazima,” na maneno kama hayo. Kwa hiyo, maneno hayo yalitumiwa mara nyingi sana katika maandishi. Katika toleo hili, vitenzi visaidizi vilidumishwa katika sehemu fulani kwa kutumia maneno kama vile “kuendelea,” na “alizoza” kulipokuwa na sababu za msingi za kuonyesha kitendo kinachoendelea. (Mwanzo 3:9; 34:1; Methali 2:4) Hata hivyo, yaliondolewa ili kurahisisha usomaji wakati vitenzi visaidizi havikuhitajiwa katika kuwasilisha maana iliyokusudiwa mwanzoni.

- **Kuwasilisha mawazo sahihi ya maneno yanayohusu jinsia.** Maneno ya Kiebrania na Kigiriki huonyesha jinsia ya kiume au ya kike, na katika Kigiriki, pia kuna maneno yasiyo na jinsia. Hata hivyo, nyakati nyingine, kuonyesha jinsia ya maneno ya lugha ya awali kunaweza kuficha maana iliyokusudiwa. Katika Kiebrania na Kigiriki, maneno yaliyo katika wingi kwa kawaida huwa na jinsia ya kiume, si yanaporejelea wanaume tu bali pia yanaporejelea wanaume na wanawake. Kwa mfano, ingawa maneno “wana wa Israeli” yanaweza kurejelea wana 12 wa Yakobo, mara nyingi hurejelea taifa zima la Israeli, wanaume na wanawake. (Mwanzo 46:5; Kutoka 35:29) Kwa hiyo, katika toleo hili, mara nyingi maneno hayo yanatafsiriwa kuwa “Waisraeli” ili kuonyesha kwamba inarejelea taifa zima. Vivyo hivyo, maneno “mvulana asiye na baba” yametafsiriwa kuwa “mtoto asiye na baba” au “yatima” ili kuonyesha kwamba yanaweza kurejelea mvulana au msichana. Kwa upande mwingine, kwa kuwa Biblia inatumia jinsia ya kiume inaporemjelea Mungu na Mwana wake, na pia malaika mbalimbali na roho waovu, hakuna msingi wa kutumia maneno yasiyo na jinsia kama inavyofanywa katika baadhi ya tafsiri za kisasa.

Marekebisho yote katika maandishi ya Biblia yalifanywa kwa sala, kwa makini, na kwa heshima kubwa kuelekea kazi nzuri iliyofanywa mwanzoni na Halmashauri ya Biblia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

Sehemu nyingine za toleo hili:

Toleo hili la Biblia lina maelezo ya chini. Kwa ujumla kuna aina zifuatazo za maelezo ya chini:

“Au”

Njia mbalimbali ambazo maandishi ya Kiebrania, Kiaramu, au Kigiriki yanaweza kutafsiriwa ili kutokeza wazo lilelile.—Mwanzo 1:2, maelezo ya chini kwenye neno “nguvu ya utendaji ya Mungu”; Yohana 1:8, “sauti ya chini.”

“Au labda”	Njia nyingine ambazo maandishi yanaweza kutaafsiriwa na kuwasilisha wazo linalokubalika lakini lililo tofauti.—Mwanzo 21:6, “atacheka pamoja nami”; Zekaria 14:21, “Mkanaani.”
“Tnn.”	Tafsiri ya neno kwa neno ya Kiebrania, Kiaramu, au Kigiriki au maana ya msingi ya maneno ya lugha ya awali.—Mwanzo 30:22, “mimba”; Kutoka 32:9, “wakaidi.”
Maana na maelezo ya ziada	Maana ya majina (Mwanzo 3:17, “Adamu”; Kutoka 15:23, “Mara”); habari kuhusu uzito na vipimo (Mwanzo 6:15, “mikono”); habari muhimu kwenye Nyongeza na Kamusi.—Mwanzo 37:35, “Kaburini”; Mathayo 5:22, “Gehena.”

Sehemu iliyo upande wa mbele, yenye kichwa “Utangulizi wa Neno la Mungu,” ina muhtasari wa mafundisho ya msingi yanayopatikana kwenye Biblia. Baada ya kitabu cha Ufunuo kuna “Orodha ya Vitabu vya Biblia,” “Fahirisi,” na “Kamusi ya Maneno ya Biblia.” Kamusi hiyo humsaidia msomaji aelewe maneno yaliyoorodheshwa humo kulingana na matumizi yake hususa katika Biblia. Nyongeza A ina sehemu zifuatazo “Kanuni za Kutafsiri Biblia,” “Sehemu za Toleo Hili,” “Jinsi Biblia Ilivyotufikia,” “Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kiebrania,” “Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo,” “Chati: Manabii na Wafalme wa Yuda na Israeli,” na “Matukio Muhimu Katika Maisha ya Yesu Duniani.” Nyongeza B ina ramani, chati, na habari nyingine muhimu kwa wanafunzi wenye bidii wa Biblia.

Kila kitabu cha Biblia kina sehemu ya yaliyomo, ambayo ina habari zilizo katika sura za kitabu hicho, pamoja na mistari hususa, na hivyo kumpa msomaji muhtasari wa kitabu chote. Sehemu ya katikati kwenye kila ukurasa ina marejeo muhimu zaidi kutoka katika matoleo yaliyotangulia, yanayoonyesha mistari ya Biblia inayohusiana.

Mtungaji na Mwanzilishi wa Biblia ndiye aliyeihifadhi pia. Yeye ndiye aliyefanya maneno haya yaa-ndikwe:

“Neno la Mungu wetu hudumu milele.”

—Isaya 40:8.

Maneno hayo ni ya kweli hata ingawa hakuna hati ya Biblia ya awali ya Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu* au Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo iliyopo leo. Kwa hiyo, tunawezaje kuwa na uhakika kabisa kwamba ujumbe ulio katika Biblia leo kwa kweli ndio uliokuwa katika maandishi ya awali yaliyoongozwa na roho ya Mungu?

WANAKILI WALILIHIFADHI NENO LA MUNGU

Kuhusu Maandiko ya Kiebrania, iliwezekana kwa sababu ya desturi ya kale iliyoanzishwa na Mungu, aliyesema kwamba maandishi yanapaswa kunakiliwa.[#] Kwa mfano, Yehova aliwaagiza wafalme wa Israeli wajiandikie nakala zao za Sheria iliyoandikwa. (Kumbukumbu la Torati 17:18) Pia, Mungu aliwapa Walawi jukumu la kuhifadhi Sheria na kuwafundisha watu kuihusu. (Kumbukumbu la Torati 31:26; Nehemia 8:7) Baada ya Wayahudi kupelekwa utekwani Babiloni, kukawa na kikundi cha wanakili, au waandishi (Wasoferi). (Ezra 7:6, maelezo ya chini) Baada ya muda, waandishi hao walitokeza nakala nyingi za vitabu 39 vya Maandiko ya Kiebrania.

Kwa karne nyingi, waandishi walinakili vitabu hivyo kwa makini. Katika Enzi za Kati, kikundi cha waandishi Wayahudi kilichoitwa Wamasora kiliendeleza desturi hiyo. Hati kamili ya kale zaidi ya Wamasora ni Kodeksi ya Leningrad, ya mwaka 1008/1009 W.K. Hata hivyo, katikati ya karne ya 20, hati 220 za Biblia au visehemu vilipatikana kati ya Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chu-

* Kuanzia hapa yanarejelewa kama Maandiko ya Kiebrania.

[#] Sababu moja iliyofanya hati zinakiliwe ni kwamba hati za awali ziliandikwa kwenye vitu vilivyoharibika haraka.

mvi. Hati hizo za Biblia ziliandikwa zaidi ya miaka 1000 kabla ya Kodeksi ya Leningrad. Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi vinapolinganishwa na Kodeksi ya Leningrad jambo muhimu linathibitika: Ingawa Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi vina tofauti fulani katika maneno, tofauti hizo haziathiri ujumbe wenyewe.

Namna gani kuhusu vile vitabu 27 vya Maandiko ya Kigiriki ya Kristo? Vitabu hivyo viliandikwa kwanza na baadhi ya mitume wa Yesu Kristo na wanafunzi wa mapema. Kwa kufuata desturi ya maandishi Wayahudi, Wakristo wa mapema walitokeza nakala za vitabu hivyo. (Wakolosai 4:16) Licha ya jitahada za Maliki Mroma Diokletiani na wengine kuharibu maandishi yote ya Wakristo wa mapema, maelfu ya visehemu na hati za kale zimehifadhiwa hadi leo.

Pia, maandishi ya Wakristo yalitafsiriwa katika lugha nyingine. Tafsiri za awali za Biblia zinatia ndani nakala za lugha za kale kama vile Kiarmenia, Kikoptiki, Kiethiopia, Kigeorgia, Kilatini, na Kisiria.

KUCHAGUA MAANDISHI YA KIEBRANIA NA YA KIGIRIKI KWA AJILI YA KUTAFSIRI

Si nakala zote za hati za kale za Biblia zilizo na maneno yanayofanana. Hivyo basi, tunawezaje kujua ujumbe uliokuwa katika hati za awali?

Hali hiyo inaweza kulinganishwa na mwalimu anayewaomba wanafunzi 100 wanakili sura fulani ya kitabu. Hata kama baadaye nakala ya awali itapotea, kulinganisha zile nakala 100 bado kunaweza kufunua ujumbe wa maandishi ya awali. Ingawa huenda kila mwanafunzi akafanya makosa, ni vigumu kwa wanafunzi wote kufanya makosa yaleyale. Vivyo hivyo, wasomi wanapolinganisha maelfu ya visehemu na nakala za vitabu vya Biblia vya kale vina vyopatikana, wanaweza kutambua makosa ya wanakili na kujua maneno yaliyokuwapo awali.

Tunawezaje kuwa na uhakika kwamba mawazo yaliyokuwa katika maandishi ya awali ya Biblia yamewasilishwa kwetu kwa usahihi? Akizungumza kuhusu maandishi ya Maandiko ya Kiebrania, msomi William H. Green alisema hivi: “Inaweza kusemwa kwa uhakika kwamba hakuna maandishi mengine ya kale yaliyowasilishwa kwa usahihi mkubwa hivyo.” Kuhusu Maandiko ya Kigiriki ya Kristo, ambayo huitwa Agano Jipya, msomi wa Biblia F. F. Bruce aliandika hivi: “Uthibitisho wa maandishi yetu ya Agano Jipya ni

“Inaweza kusemwa kwa uhakika kwamba hakuna maandishi mengine ya kale yaliyowasilishwa kwa usahihi mkubwa hivyo”

Sura ya 40 ya kitabu cha Isaya katika Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi (ya mwaka wa 125 mpaka 100 K.W.K.)

Yanapolinganishwa na hati za Kiebrania zilizoandikwa miaka elfu moja baadaye, kuna tofauti ndogo tu, hasa katika kuandika maneno



Sura ya 40 ya kitabu cha Isaya katika Kodeksi ya Aleppo, hati muhimu ya Kiebrania ya Wamasora ya karibu mwaka wa 930 W.K.



mkubwa zaidi kuliko uthibitisho wa maandishi mengi ya waa-ndikaji wa kale, na hakuna mtu anayeweza kutilia shaka usahihi wake.” Pia anasema: “Ikiwa Agano Jipya lingekuwa mkusanyo wa maandishi ya kilimwengu, usahihi wake haungetiliwa shaka kamwe.”

Maandishi ya Kiebrania: *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya ya Maandiko ya Kiebrania* katika Kiingereza (1953-1960) ilitengemea *Biblia Hebraica*, ya Rudolf Kittel. Tangu wakati huo, matoleo yaliyoboreshwa ya maandishi ya Kiebrania, yaani, *Biblia Hebraica Stuttgartensia* na *Biblia Hebraica Quinta*, yameongeza utafiti wa karibuni unaotegemea Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi na hati nyingine za kale. Maandishi hayo ya wasomi yanafanana na Kodeksi ya Leningrad na yana maelezo ya chini yaliyo na maneno yenye ulinganifu kutoka vyanzo vingine, kutia ndani Pentateuki ya Samaria, Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi, *Septuajinti* ya Kigiriki, Targumi za Kiaramu, *Vulgate* ya Kilatini, na *Peshitta* ya Kisiria. *Biblia Hebraica Stuttgartensia* na *Biblia Hebraica Quinta* zilitumiwa katika kuandaa toleo hili la *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

Maandishi ya Kigiriki: Mwishoni mwa karne ya 19, msomi B. F. Westcott na F.J.A. Hort walilinganisha hati za Biblia na visehemu vilivyokuwapo walipokuwa wakiandaa maandishi ya Kigiriki ambayo walihisi yalikaaribiana zaidi na maandishi ya awali. Katikati ya karne ya 20 Halmashauri ya Biblia ya Tafsiri ya Ulimwengu Mpya ilitumia maandishi hayo kama msingi wa tafsiri yao. Pia, walitumia mafunjo mengine ya kale, yanayodhaniwa kuwa ya karne ya pili au ya tatu W.K. Tangu wakati huo, mafunjo mengi zaidi yamepatikana. Isitoshe, maandishi kama yale ya Nestle na Aland na ya *United Bible Societies* yana utafiti wa karibuni zaidi wa wasomi. Baadhi ya habari zilizo katika utafiti huo zimetumiwa katika toleo hili.


Kwa msingi wa maandishi hayo, ni wazi kwamba baadhi ya mistari katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo iliyokuwa katika tafsiri za zamani, kama vile *King James Version*, kwa kweli ilikuwa imeongezwa na wanakili wa baadaye na haikuwa kamwe sehemu ya Maandiko yaliyoongozwa na roho ya Mungu. Hata hivyo, kwa kuwa kugawanywa kwa mistari ambako kwa kawaida kuna kubalika katika tafsiri za Biblia tayari kulikuwa kumeanzishwa katika karne ya 16, kuondolewa kwa mistari hiyo huacha mapengo katika mistari fulani ya Biblia nyingi. Mistari hiyo ni Mathayo 17:21; 18:11; 23:14; Marko 7:16; 9:44, 46; 11:26; 15:28; Luka 17:36; 23:17; Yohana 5:4; Matendo 8:37; 15:34; 24:7; 28:29; na Waroma 16:24. Katika toleo hili lililorekebishwa, mistari hiyo iliyoondolewa ina maelezo ya chini mahali inapopatikana.

Kuhusu umalizio mrefu wa Marko 16 (mistari ya 9-20), umalizio mfupi wa Marko 16, na maneno yaliyo kwenye Yohana 7:53–8:11, ni wazi kwamba mistari hiyo haikuwa katika hati za awali. Kwa hiyo, maandishi hayo yaliyoongezwa hayajawekwa kwenye toleo hili.*

Baadhi ya maneno yamerekebishwa ili kutia ndani mawazo ambayo kwa kawaida wasomi huyakubali kuwa mawazo sahihi zaidi ya maandishi ya awali. Kwa mfano, kulingana na baadhi ya hati, andiko la Mathayo 7:13 linasema: “Ingieni kupitia lango jembamba, kwa sababu lango ni pana, na barabara inayoongoza kwenye uharibifu ina nafasi kubwa.” Katika matoleo yaliyotangulia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*, maneno “lango ni” hayakuwapo. Hata hivyo, uchunguzi zaidi wa hati ulithibitisha kwamba maneno “lango ni” yalikuwa katika maandishi ya awali. Basi yalitiwa ndani kwenye toleo hili. Kuna marekebisho mengine kama hayo. Hata hivyo, marekebisho hayo ni madogo, na hayabadili ujumbe wa msingi wa Neno la Mungu.

* Habari zaidi kuhusu kwa nini mistari hiyo inaonwa kuwa ya kuongezwa inaweza kupatikana kwenye maelezo ya chini ya *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*—Yenye Marejezo katika Kiingereza ya mwaka 1984.

Hati ya mafunjo ya
2 Wakorintho 4:13–5:4
ya karibu mwaka wa
200 W.K.



Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kiebrania

Jina la Mungu, linalowakilishwa na konsonanti nne za Kiebrania יהוה, linapatikana karibu mara 7,000 katika Maandiko ya Kiebrania. Katika tafsiri hii herufi hizo nne, zinazojulikana kama Tetragramatoni, zimetafsiriwa kuwa “Yehova.” Hilo ndilo jina linalopatikana mara nyingi zaidi katika Biblia. Ingawa waandikaji walioongozwa na roho takatifu walimtaja Mungu kwa kutumia majina ya cheo, kama vile “Mweza-Yote,” “Aliye Juu Zaidi,” na “Bwana,” walitumia hasa Tetragramatoni kuandika jina binafsi la Mungu.

Yehova Mungu ndiye aliyewaongoza waandikaji wa Biblia kutumia jina lake. Kwa mfano, alimwongoza nabii Yoeli kuandika hivi: “Kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokolewa.” (Yoeli 2:32) Na Mungu alimtumia mtungazaburi mmoja kuandika: “Na watu wajue kwamba wewe, ambaye jina lako ni Yehova, wewe peke yako ndiye Uliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote.” (Zaburi 83:18) Kwa kweli, jina la Mungu linapatikana mara 700 hivi katika kitabu cha Zaburi peke yake—ambacho ni kitabu chenye maandishi ya ushairi yaliyoimbwa na kukaririwa na watu wa Mungu. Basi, kwa nini tafsiri nyingi za Biblia hazina jina la Mungu? Kwa nini tafsiri hii imetumia jina “Yehova”? Na jina la Mungu, Yehova, linamaanisha nini?

Kwa nini jina hilo halipatikani katika tafsiri nyingi za Biblia? Kuna sababu mbalimbali. Watu fulani husema kwamba Mungu Mweza-Yote hapaswi kutambulishwa kwa jina la kipekee. Wengine wanafuata desturi ya Kiyahudi ya kutolitumia jina hilo, labda kwa kuogopa kulikufuru. Nao wengine wanaamini kwamba kwa kuwa hakuna mtu anayejua kikamili jinsi jina la Mungu lilivyotamkwa, ni afadhali kutumia jina la cheo, kama vile “Bwana” au “Mungu.” Hata hivyo, maoni hayo hayana msingi kwa sababu zifuatazo:

- Wale wanaodai kwamba Mungu Mweza-Yote hapaswi kutambulishwa kwa jina la kipekee wanapuuza uthibitisho wa kwamba nakala za awali za Neno lake, kutia ndani nakala

יהוה

Jina la Mungu katika herufi za kale za Kiebrania zilizotumiwa kabla ya Wayahudi kwenda utekwani Babiloni

יהוה

Jina la Mungu katika herufi za Kiebrania zilizotumiwa baada ya Wayahudi kutoka utekwani Babiloni

וּבְרִיךְ שֵׁם לַאֲלֹהֵי וַעַד כְּלִמְתֻכָּהּ לִסְתֵּר כּוֹל עֲלֵפוֹת וּבְנֵי אֲדָמָה
כָּל אֲדָרָה וְיָהּ בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד נִסְתָּר
אֱלֹהִים בְּרִיךְ וְחֲסוּד כָּל עֲשֵׂה בְרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד
שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד סוֹכֵךְ לְכֹל אֲנֵי כְּלֵס וּוְדָר לְכֹל
חֲכִמִּים בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד עֵינַי
כֹּל אֱלֹהִים וְשִׁיר וְיָהּ עֵינַי לְכֹחַ אֱלֹהֵי כְּעֵינַי
בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד כִּתְּמָה אִתָּה אֵת
וְיָהּ וְנִשְׁמַע לְכֹל אֲרִמְנוֹן בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד
לַאֲלֵהֵי וַעַד בְּרִיךְ אֱלֹהֵי כָּל אֲרִמְנוֹן וְחֲסוּד כָּל
עֲשֵׂה בְרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד קִיּוֹם
וְרִיךְ שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד וְקִיּוֹמוֹ כִּימְנוֹת בְּרִיךְ אֱלֹהֵי
וְרִיךְ שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד יֵעֹן וְיָהּ וְעֵשָׂה וְאֵת אֲוֵעַתְּכֵי
אֲנֵי וְיָהּ שֵׁם לַאֲלֵהֵי וַעַד בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד
סוֹכֵךְ אֵת כָּל וְיָהּ וְיָהּ וְיָהּ וְיָהּ וְיָהּ וְיָהּ
בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד
בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד בְּרִיךְ אֱלֹהֵי וַעַד

Maandishi ya Zaburi ya Kitabu cha Kukunjwa cha Bahari ya Chumvi yaliyoandikwa mwanzoni mwa karne ya kwanza W.K. Maandishi hayo yameandikwa kwa kutumia herufi za Kiebrania zilizotumiwa baada ya Wayahudi kutoka utekwani Babiloni, lakini Tetragramatoni imeandikwa waziwazi tena na tena kwa herufi za kale za Kiebrania


zilizohifadhiwa tangu enzi za kabla ya Kristo, zina jina binafsi la Mungu. Kama ilivyotajwa hapo juu, Mungu aliwaongoza waadikaji kuandika jina lake mara 7,000 hivi katika Neno lake. Bila shaka, anataka tulijue na kulitumia jina lake.

- Watafsiri wanaoondoa jina hilo kwa kufuata desturi ya Kiyahudi wanakosa kuelewa jambo fulani muhimu. Ingawa waandishi fulani Wayahudi waliepuka kulitamka jina hilo, hawakuliondoa kwenye nakala zao za Biblia. Vitabu vya kukunjwa vya kale vilivyopatikana huko Qumran, karibu na Bahari ya Chumvi, vina jina hilo katika sehemu nyingi. Watafsiri fulani wa Biblia wana-dokeza kwamba jina la Mungu lilipatikana katika maandishi ya awali kwa kuandika jina la cheo “BWANA” kwa herufi kubwa. Lakini huenda tukajjuliza, Kwa nini watafsiri hao waliamua kutumia jina la cheo au kuondoa jina la Mungu katika Biblia ingawa wanakubali kwamba linapatikana katika maandishi ya Biblia mara nyingi? Ni nani aliyewapa mamlaka ya kufanya mabadiliko hayo? Wao ndio wanaojua.
- Wale wanaosema kwamba jina la Mungu halipaswi kutumiwa kwa sababu haijulikani hasa jinsi lilivyotamkwa, wanatumia jina la Yesu kwa uhuru. Hata hivyo, wanafunzi wa Yesu katika karne ya kwanza walitamka jina lake tofauti na jinsi Wakristo wengi wanavyolitamka leo. Huenda Wakristo Wayahudi walilitamka jina Yesu, *Ye-shu’a*. Na kuhusu jina la cheo “Kristo” walitumia *Ma-shi’ach*, au “Masihi.” Wakristo waliozungumza Kigiriki walimwita *I-e-sous’ Khri-stos’*, na Wakristo waliozungumza Kilatini walimwita *le’sus Chri’stus*. Kwa mwongozo wa roho takatifu, tafsiri ya Kigiriki ya jina lake iliandikwa katika Biblia, na hivyo kuonyesha kwamba Wakristo wa karne ya kwanza walitumia busara kwa kutumia jina lililotumiwa na watu wengi katika lugha yao. Vivyo hivyo, Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya inaamini kwamba ni jambo la busara kutumia jina “Yehova,” ingawa huenda jina la Mungu lilitamkwa kwa njia tofauti katika Kiebrania cha kale.

Kwa nini Tafsiri ya Ulimwengu Mpya inatumia jina “Yehova”? Katika Kiswahili, herufi nne za Tetragramatoni (יהוה) zinawakilishwa na konsonanti *YHWH*. Kama ilivyokuwa na maneno yote yaliyoandikwa katika Kiebrania cha kale, Tetragramatoni haikuwa na vokali. Katika matamshi yao ya kawaida, wasomaji wa Kiebrania cha kale waliongeza vokali zifaazo.

Karibu miaka elfu moja baada ya Maandiko ya Kiebrania kukamilishwa, wasomi Wayahudi walibuni alama za matamshi, au ishara, ambazo zilionyesha vokali zilizotumiwa kusoma Kiebrania. Hata hivyo, wakati huo Wayahudi wengi walikuwa na mawazo

Jina la Mungu
kwenye Mwanzo
15:2 katika tafsiri
ya William Tyndale
ya Pentateuki, 1530



ya kishirikina kwamba ni makosa kutaja jina la Mungu kwa sauti, basi walitumia majina ya badala. Hivyo, inaonekana kwamba waliponakili Tetragramatoni, waliunganisha vokali za *majina* ya *badala* pamoja na zile konsonanti nne zinazowakilisha jina la Mungu. Kwa hiyo, hati za awali zenye alama hizo za matamshi haziwezi kutusaidia kujua jinsi jina hilo lilivyotamkwa mwanzoni katika Kiebrania. Watu fulani husema kwamba jina hilo lilitamkwa “Yahweh,” huku wengine wakiwa na maoni tofauti. Kitabu fulani cha kukunjwa cha Bahari ya Chumvi kina kisehemu cha kitabu cha Mambo ya Walawi cha Kigiriki kilichotohoa jina la Mungu kuwa *lao*. Zaidi ya kutumia *lao*, waandikaji wa kale wa Kigiriki wanadokeza pia matamshi kama *lae*, *l-a-be’*, na *l-a-ou-e’*. Hata hivyo hakuna sababu ya kuweka sheria. Kwa kweli hatujui jinsi watumishi wa kale wa Mungu walivyotamka jina hili katika Kiebrania. (Mwanzo 13:4; Kutoka 3:15) Tunachojua ni kwamba Mungu alitumia jina lake mara nyingi alipozungumza na watu wake, na kwamba walimwita kwa kutumia jina hilo, na walilitumia kwa uhuru katika mazungumzo yao.—Kutoka 6:2; 1 Wafalme 8:23; Zaburi 99:9.

Hivyo basi, kwa nini tafsiri hii inatumia jina “Yehova”? Kwa sababu jina hilo la Mungu limetumiwa kwa miaka mingi sana katika lugha ya Kiswahili.

Pia, jina hilo limeandikwa kwa njia mbalimbali katika lugha nyingine, kwa mfano, jina la Mungu lilitumiwa kwa mara ya kwanza katika Biblia ya Kiingereza mwaka wa 1530 katika tafsiri ya William Tyndale ya Pentateuki. Alitumia jina “*Iehouah*.” Baada ya muda, lugha ya Kiingereza ilibadilika, na herufi za jina la Mungu zikaboreshwa. Kwa mfano, mwaka wa 1612, Henry Ainsworth alitumia jina “*Iehovah*” alipotafsiri kitabu chote cha Zaburi. Kisha, mwaka wa 1639, tafsiri hiyo ilipofanyiwa marekebisho na kuchapishwa pamoja na Pentateuki, jina “*Iehovah*” lilitumiwa. Mwaka

wa 1901, watafsiri waliotokeza Biblia ya *American Standard Version* walitumia jina “*Jehovah*” mahali palipokuwa na jina la Mungu katika maandishi ya Kiebrania.

Akieleza sababu iliyofanya atumie jina “*Jehovah*” badala ya “*Yahweh*” katika kitabu chake *Studies in the Psalms*, cha 1911, msomi aliyeheshimiwa wa Biblia Joseph Bryant Rotherham alisema kwamba alitaka kutumia “jina ambalo lilitumiwa zaidi (na kukubaliwa kabisa) na wasomaji wengi wa Biblia.” Mwaka wa 1930 msomi A. F. Kirkpatrick alisema jambo kama hilo kuhusu matumizi ya jina “*Jehovah*.” Alisema hivi: “Wasomi wa kisasa wa lugha wanaidai kwamba linapaswa kuandikwa *Yahveh* au *Yahaveh*; lakini inaonekana *JEHOVAH* ndilo linalotumika zaidi katika Kiingereza, na jambo muhimu si kujua matamshi kamili, bali kutambua kwamba ni Jina Binafsi, tofauti na jina la cheo kama vile ‘Bwana.’” Katika Biblia nyingi za Kiswahili, jina la Mungu huandikwa “*Yehova*.”

Jina Yehova linamaanisha nini? Katika Kiebrania, jina Yehova linatokana na kitenzi kinachomaanisha “kuwa,” na wasomi fulani wanafikiri kwamba ni kitenzi kisababishi katika lugha ya Kiebrania. Hivyo basi, kulingana na Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya jina la Mungu linamaanisha “*Yeye Husababisha Kuwa*.” Wasomi wana maoni mbalimbali, na hivyo hatuwezi kusisitiza maana hiyo. Hata hivyo, ufafanuzi huo unafaa kabisa kuhusiana na jukumu la Yehova akiwa Muumba wa vitu vyote na Mtimizaji wa kusudi lake. Mbali na kuumba ulimwengu na viumbe wenye akili, kadiri muda unavyosonga, ndivyo anavyoendelea kutimiza mapenzi na kusudi lake.

Kwa hiyo, maana ya jina Yehova haihusiani tu na kitenzi kilicho kwenye andiko la Kutoika 3:14 linalosema: “Nitakuwa Kile Ninachochagua Kuwa” au “Nitathibitika Kuwa Kile Nitakachothibitika Kuwa.” Ukweli ni kwamba maneno hayo ni sehemu tu ya maana kamili ya jina la Mungu. Yaani, yanafunua jambo fulani kuhusu utu wa Mungu, ya kionyesha kwamba yeye huwa chochote kinachohitajika katika kila hali ili kutimiza kusudi lake. Kwa hiyo, ingawa huenda jina Yehova linatia ndani maana hiyo, jina hilo halimaanishi tu kile anachoamua kuwa. Pia, linatia ndani mambo anayosababisha yatendeke kuhusiana na uumbaji wake na kutimizwa kwa kusudi lake.

יהוה

Tetragramatoni,
YHWH: “*Yeye
Husababisha
Kuwa*”

יהוה

Kitenzi *HWH*:
“*kuwa*”

Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo

Wasomi wa Biblia wanakubali kwamba jina binafsi la Mungu, linalowakilishwa na Tetragramatoni (יהוה), linapatikana karibu mara 7,000 katika maandishi ya awali ya Maandiko ya Kiebrania. Hata hivyo, wengi wanahisi kwamba halikupatikana katika maandishi ya awali ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Kwa hiyo, tafsiri nyingi za kisasa za Biblia ya Kiswahili hazitumii jina Yehova katika sehemu inayoitwa Agano Jipya. Hata wanapotafsiri sehemu zilizonukuliwa za Maandiko ya Kiebrania ambapo Tetragramatoni ilipatikana, watafsiri wengi hutumia jina “Bwana” badala ya jina binafsi la Mungu.

Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya haifuati mtindo huo wa kutafsiri. Inatumia jina Yehova mara 237 katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Walipoamua kufanya hivyo, watafsiri walifikiria mambo mawili muhimu: (1) Hati za Kigiriki tulizo nazo leo si hati za awali kabisa. Kati ya maelfu ya nakala zilizopo leo, nyingi ziliandikwa miaka mia mbili hivi baada ya nakala za kwanza kuandikwa. (2) Wakati huo, wale walionakili hati za kale walibadili Tetragramatoni na kutumia *Ky’ri-os*, neno la Kigiriki linaloamaanisha “Bwana,” au walinakili kutoka kwa hati ambazo tayari zilikuwa zimebadili jina la Mungu.

Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya iliamua kwamba kuna uthibitisho wa kutosha kuwa Tetragramatoni ilipatikana katika hati za awali za Kigiriki. Uamuzi huo ulitegemea uthibitisho ufuatao:

- **Nakala za Maandiko ya Kiebrania zilizotumiwa katika siku za Yesu na mitume wake zilikuwa na Tetragramatoni kote kote katika Maandiko.** Zamani watu fulani walipinga hoja hiyo. Kwa kuwa sasa nakala za Maandiko ya Kiebrania zilizoandikwa katika karne ya kwanza zimepatikana karibu na Qumran, jambo hilo limethibitishwa kikamili.
- **Katika siku za Yesu na mitume wake, Tetragramatoni ilipatikana pia katika tafsiri za Kigiriki za Maandiko ya Kiebrania.** Kwa karne nyingi, wasomi walifikiri kwamba Tetragramatoni haikupatikana katika hati za Septuajinti, yaani, tafsiri ya Kigiriki ya Maandiko ya Kiebrania. Kisha, katikati ya karne ya 20, wasomi walipata vipande fulani vya kale sana vya Septuajin-

ti ya Kigiriki ambavyo vilitumiwa katika siku za Yesu. Vipande hivyo vina jina binafsi la Mungu, likiwa limeandikwa kwa herufi za Kiebrania. Basi katika siku za Yesu, nakala za Maandiko ya Kigiriki zilikuwa na jina la Mungu. Hata hivyo, kufikia karne ya nne W.K., hati kuu za *Septuajinti* ya Kigiriki, kama vile Kodeksi ya Vatikani na Kodeksi ya Sinai, hazikuwa na jina la Mungu kuanzia kitabu cha Mwanzo hadi Malaki (ingawa hati za awali zilikuwa na jina hilo). Hivyo, haishangazi kuona kwamba nakala zilizohifadhiwa za wakati huo, hazina jina la Mungu katika sehemu inayoitwa Agano Jipya, au Maandiko ya Kigiriki katika Biblia.

- **Maandiko ya Kigiriki yanaripoti kwamba Yesu alitumia jina la Mungu mara nyingi na kuwajulisha wengine kulihusu.** (Yohana 17:6, 11, 12, 26) Yesu alisema hivi waziwazi: “Nimekuja katika jina la Baba yangu.” Pia, alikazia kwamba alifanya kazi katika “jina la Baba” yake.—Yohana 5:43; 10:25.
- **Kwa kuwa Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo yaliyoongozwa na roho ya Mungu yaliiongezwa kwenye Maandiko matakatiifu ya Kiebrania, haingewezekana jina la Mungu liondolewe ghafula.** Katika karne ya kwanza W.K., mwanafunzi Yakobo aliwaambia hivi wazee huko Yerusalemu: “Simioni amesimulia kikamili jinsi Mungu kwa mara ya kwanza alivyoelekeza uangalifu wake kwa mataifa ili achukue kutoka kwao watu kwa ajili ya jina lake.” (Matendo 15:14) Yakobo hangesea maneno hayo ikiwa hakuna mtu yeyote katika karne ya kwanza ambaye alijua au kutumia jina la Mungu.
- **Jina la Mungu limeandikwa kwa ufupisho katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.** Kwenye andiko la Ufunuo 19:1, 3, 4, 6, jina la Mungu linapatikana katika neno “Haleluya.” Neno hilo linatokana na maneno ya Kiebrania yanayomaanisha “Msifuni Yah.” “Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. Majina mengi yaliyotumiwa katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo yalitokana na jina la Mungu. Kwa kweli, utafiti unaonyesha kwamba jina Yesu linamaanisha “Yehova Ni Wokovu.”
- **Maandishi ya kale ya Wayahudi yanaonyesha kwamba Wakristo Wayahudi walitumia jina la Mungu katika maandishi yao.** Mkusanyo wa sheria unaoitwa *Tosefta*, ambao ulikamilishwa

Yesu alisema hivi waziwazi: “Nimekuja katika jina la Baba yangu.” Pia, alikazia kwamba alifanya kazi katika “jina la Baba” yake

300

200

100

K.W.K. ← | → W.K.

100



Kumbukumbu la Torati 6:4
Mafunjo ya Nash
Karne ya pili au ya kwanza K.W.K.



Kisehemu cha Kumbukumbu la Torati 18:15, 16
P. Fouad Inv. 266
Karne ya kwanza K.W.K.

Maandishi ya kale ya Kiebrania
yenye jina la Mungu mara mbili

Tafsiri ya Septuajinti ya Kigiriki
ikiwa na jina la Mungu katika
herufi za Kiebrania

karibu mwaka wa 300 W.K., unasema hivi kuhusu maandishi ya Wakristo yaliyoteketezwa siku ya Sabato: “Wanaviteketeza vitabu vya Waeneza Injili na vitabu vya *minim* [watu wanaodhaniwa kuwa Wakristo Wayahudi]. Vinateketezwa popote vinapopatikana, pamoja na marejeo ya Jina la Mungu lililo katika vitabu hivyo.” Maandishi hayo pia yanamnukuu Mgalilaya anayeitwa Rabi Yosé aliyeishi mwanzoni mwa karne ya pili W.K., akisema kwamba katika siku nyingine za juma “mtu hukata marejeo ya Jina la Mungu [katika maandishi ya Kikristo] na kuyahifadhi, kisha anateketeza maandishi yanayobaki.”

300

400

500

1900

1950

2000

ΚΕΝΙΚΟΘΘΘΟΥΙ
 ΛΧΕΑΧΘΩΝΙΟΥ
 ΟΙΚΕΘΘΘΟΥΑΥ
 ΚΑΤΑΠΑΝΤΑΘΕΑΓΙ
 ΘΥΣΟΥΘΗΧΩΡΗ

ΑΘΘΘΕΜΘΑΧΘΗΘ
 ΚΥΤΟΥΑΚΟΥΘΘΘ
 ΗΓΓΙΘΘΗΑΡΧΥΘ
 ΗΚ'ΤΗΜΕΡΑΘΗΘ
 ΘΟΝΤΕΘΟΥΗΡΟΘ

...ome^o from the person of Je-
 he may send forth the Christ^a
 , Jesus, ²¹ whom heaven, in-
 within itself^b until the times
 all things of which God spoke
 of his holy prophets^o of old
 oses said: 'Jehovah^c God will
 rom among YOUR brothers a
 OU must listen to him accord-
 s he speaks to YOU.^x ²³ Indeed,
 s not listen to that Prophet
 destroyed from among the
 the prophets, in fact, from

Kumbukumbu la Torati 18:15, 16
 Kodeksi ya Alexandria
 Karne ya tano W.K.

Andiko la Matendo 3:22, likinukuu
 Kumbukumbu la Torati 18:15
 Tafsiri ya Ulimwengu Mpya
 Karne ya 20 W.K.


Jina la Mungu likiwa
 limeondolewa na badala yake
 kuwekwa herufi KC na KY,
 ambao ni ufupisho wa neno
 la Kirigiki Ky'ri-os (Bwana)

Tafsiri ya Ulimwengu Mpya
 imerudisha jina la Mungu

- Baadhi ya wasomi wa Biblia wanasema inawezekana kwamba jina la Mungu lilipatikana katika Maandiko ya Kigiriki ya Ki-kristo kwenye sehemu zilizonukuu Maandiko ya Kiebrania. Kamusi ya *The Anchor Bible Dictionary* chini ya kichwa "Tetragramatoni Katika Agano Jipya," inasema: "Kuna uthibitisho kwamba, maandishi ya Agano Jipya yalipoandikwa kwa mara ya kwanza, Tetragramatoni, Jina la Mungu, Yahweh, ilipatikana katika baadhi au sehemu zote za Agano la Kale zilizonukuliwa katika Agano Jipya." Msomi George Howard anasema hivi: "Kwa kuwa bado Tetragramu iliandikwa katika nakala za Biblia ya Kigiriki [Septuajinti] iliyofanyiza Maandiko ya kanisa

la awali, ni jambo la busara kuamini kwamba waandishi wa Agano Jipya walitumia Tetragramu katika Biblia waliponukuu Maandiko.”

- **Watafsiri maarufu wa Biblia wametumia jina la Mungu katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.** Baadhi ya watafsiri hao walifanya hivyo muda mrefu kabla ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* kuchapishwa. Tafsiri hizo zinatia ndani *A Literal Translation of the New Testament . . . From the Text of the Vatican Manuscript*, ya Herman Heinfetter (1863); *The Emphatic Diaglott*, ya Benjamin Wilson (1864); *The Epistles of Paul in Modern*




Jina la Mungu kwenye Matendo 2:34 katika tafsiri ya *The Emphatic Diaglott*, ya Benjamin Wilson (1864)

English, ya George Barker Stevens (1898); *St. Paul's Epistle to the Romans*, ya W. G. Rutherford (1900); *The New Testament Letters*, ya J.W.C. Wand, Askofu wa London (1946). Isitoshe, katika tafsiri ya Kihispania mwanzoni mwa karne ya 20, mtafsiri Pablo Besson alitumia jina “*Jehová*” kwenye Luka 2:15 na Yuda 14, na zaidi ya mara 100 katika maelezo ya chini ya tafsiri yake. Muda mrefu kabla ya tafsiri hizo, tafsiri za Kiebrania za Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo kuanzia karne ya 16 na kuendelea zilitumia Tetragramatoni katika sehemu nyingi. Katika Kijerumani peke yake, karibu tafsiri 11 zinatumia jina

“Yehova” (au “Yahweh” kama linavyotoholewa kutoka katika Kiebrania) katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, na watafsiri wanne waliongeza jina hilo katika mabano baada ya jina “Bwana.” Zaidi ya tafsiri 70 za Kijerumani zinatumia jina la Mungu katika maelezo ya chini au katika marejeo.

- **Tafsiri za Biblia katika lugha zaidi ya 100 zina jina la Mungu katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.** Lugha nyingi za Afrika, za wenyeji wa asili wa Amerika, Asia, Ulaya, na visiwa vya Pasifiki zinatumia jina la Mungu mara nyingi. (Ona orodha iliyo kwenye ukurasa wa 2062 na 2063.) Watafsiri wa matoleo hayo waliamua kutumia jina la Mungu kwa sababu zinazofanana na zile zilizotajwa hapo juu. Baadhi ya tafsiri hizo za Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo zimechapishwa hivi karibuni, kama vile Biblia ya Kiroduma (1999), inayotumia jina “*Jihova*” mara 51 katika mistari 48, na tafsiri ya Batak (Toba) ya Indonesia (1989), inayotumia jina “*Jahowa*” mara 110.

Bila shaka, kuna msingi thabiti wa kurudisha jina la Mungu, Yehova, katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Hivyo ndivyo walivyofanya watafsiri wa Biblia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*. Wanalishimu sana jina la Mungu na kwa kufaa wanaogopa kuondoa chochote kilichokuwa kimeandikwa katika maandishi ya awali. —Ufunuo 22:18, 19.



Jina la Mungu kwenye Marko 12:29, 30 katika tafsiri ya Kihawaii

Lugha na Lahaja Zilizo na Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo

Lugha au Lahaja: Jina la Mungu

Kianeityum: Ihova	Kiholanzi: Jehovah
Kiarawak: Jehovah	Kiila: Yaave
Kiawabakal: Yehôa	Kiiliku (lahaja ya Kilusengo): Yawe
Kibangi: Yawe	Kiindonesia: YAHWEH
Kibatak (Toba): Jahowa	Kiingereza: Jehovah
Kibenga: Jêhova	Kijaluo: Yawe
Kibolia: Yawe	Kijerumani: Jehovah; Jehova
Kibube: Yehovan	Kikala Lagaw Ya: lehovan
Kibullom So: Jehovah	Kikalanga: Yehova; Yahwe
Kichácobo: Jahué	Kikalenjin: Jehovah
Kicherokee: Yihowa	Kikerewo: lehova
Kichin (Hakha): Zahova	Kikorea: 여호와
Kichippewa: Jehovah	Kikosrae: Jeova
Kichoctaw: Chihowa	Kikroatia: Jehova
Kichuukese: Jiowa	Kikuanua: leova
Kidakota: Jehowa	Kilaotia: Yehowa
Kidobu: leoba	Kilele: Jehova
Kidouala: Yehowa	Kilewo: Yehova
Kiebrania: יהוה	Kilogo: Yehova
Kiefate (Kaskazini): Yehova	Kilomongo: Yawe; Yova
Kiefik: Jehovah	Kilonwolwol: Jehovah
Kiéwé: Yehowa	Kiluba: Yehova
Kifang: Jehôva	Kilugbara: Yehova
Kifaransa: IHVH, yhwh	Kiluimbi: Yehova
Kifiji: Jiova	Kiluna: Yeoba
Kiga: lehova	Kilunda: Yehova
Kigibario (lahaja ya Kikerewo): lehova	Kiluvale: Yehova
Kigrebo: Jehova	Kimalagasi: Jehovah; lehôvah
Kihawaii: lehova	Kimalo: Iova
Kihindustani: Yihováh	Kimarquesa: lehova
Kihiri Motu: lehova	Kimarshall: Jeova
Kihispania: Jehová; Yahvé; YHWH; Yahweh	Kimaskelyne: Iova
Kiho-Chunk (Winnebago): Jehowa	Kimentawai: Jehoba
	Kimeriam: lehoua

Kimisima-Paneati: **Iehova**
Kimizo: **Jehovan; Jihova'n**
Kimohawk: **Yehovah**
Kimortlock: **Jioua**
Kimotu: **Iehova**
Kimpongwe (lahaja ya Kimyene): **Jehova**
Kimuskoge: **Cehofv**
Kimyene: **Yeôva**
Kinaga, Kiangami: **Jihova**
Kinaga, Kikonyak: **Jihova**
Kinaga, Kilotha: **Jihova**
Kinaga, Kimao: **Jihova**
Kinaga, Rengma Kaskazini: **Jihova**
Kinaga, Sangtam: **Jihova**
Kinandi: **Jehova**
Kinarrinyeri: **Jehovah**
Kinauru: **Jehova**
Kinavajo: **Jiho'vah**
Kindau: **Jehova**
Kinembe: **Jehovah**
Kinengone (au, Kimarê): **Iehova**
Kingala: **Yawe**
Kingando: **Yawe**
Kintomba: **Yawe**
Kinukuoro: **Jehova**
Kipolandi: **Jehowa**
Kipsigis: **Jehoba**
Kirarotonga: **Jehova; Iehova**
Kireno: **Iáhve**
Kirerep: **Iova**
Kiribati: **Iehova**
Kirotuman: **Jihova**
Kisakao: **Ihova; Iehova**
Kisamoa: **Ieova**


Kiseneka: **Ya'wën**
Kisengele: **Yawe**
Kisesotho: **Yehofa**
Kisie: **Iehôva**
Kisonge: **Yehowa**
Kisranantongo: **Jehova**
Kisukuma: **Yahuwa; Jakwe**
Kitahiti: **Iehova**
Kiteke-Eboo: **Yawe**
Kitemne: **Yehôfa; Yehofa**
Kithai: **Yahowa**
Kitoaripi: **Jehova; Iehova**
Kitonga: **Jehova**
Kitongan: **Jihova; Sihova**
Kitshiluba: **Yehowa**
Kitswana: **Jehofa; Yehova; Yehofa**
Kiumbundu: **Yehova**
Kiuripiv: **Iova**
Kiwapanoag: **Jehovah**
Kiwelsh: **Iehofah**
Kixhosa: **Yehova**
Kizande: **Yekova**
Kizulu: **Jehova; YAHWE**

(Lugha na lahaja nyingine zisizo kwenye orodha hii hutumia jina la Mungu kwenye maelezo ya chini au kwenye maandishi ya ufafanuzi.)


Zaidi ya lugha 120

Chati: Manabii na Wafalme wa Yuda na Israeli

Wafalme wa Ufalme wa **Kusini** wa Yuda
Uliokuwa na Makabila Mawili



Wafalme wa Ufalme wa **Kaskazini** wa Israeli Uliokuwa na Makabila Kumi



Wafalme wa Ufalme wa Kusini
(Imeendelezwa)

Uzia (Azaria): Miaka 52

777

Yothamu: Miaka 16

762

Ahazi: Miaka 16

746

Hezekia: Miaka 29

716

Manase: Miaka 55

661

Amoni: Miaka 2

659

Yosia: Miaka 31

628

Yehoahazi: Miezi 3

618

Yehoyakimu: Miaka 11

617

Yehoyakini: Miezi 3, siku 10

607

Sedekia: Miaka 11

Jiji la Yerusalemu na hekalu lake laharibiwa na majeshi ya Wababiloni yakiongozwa na Nebukadneza. Sedekia, mfalme wa mwisho wa kidunia katika ukoo wa Daudi, aondolewa mamlakani

800 K.W.K.

Mika

Isaya

750 K.W.K.

700 K.W.K.

Nahumu

Yeremia

Sefania

Habakuki


Obadia

Ezekieli

Danieli

Wafalme wa Ufalme wa Kaskazini
(Imeendelezwa)

Hosea



650 K.W.K.

600 K.W.K.

Matukio Muhimu Katika Maisha ya Yesu Duniani

Vitabu Vinne vya Injili Kulingana na Mfuatano wa Matukio

Chati zifuatazo zina ramani zinazoonyesha safari za kuhubiri za Yesu. Mishale kwenye ramani haionyeshi njia hususa aliyofuata badala yake inaonyesha alikoelekea.

Matukio Yaliyotangulia Huduma ya Yesu


WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
3 K.W.K.	Yerusalemu, hekalu	Malaika Gabrieli amtangazia Zekaria kuhusu kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji	
Karibu 2 K.W.K.	Nazareti; Yudea	Malaika Gabrieli amtangazia Maria kuhusu kuzaliwa kwa Yesu; Maria amtembelea Elisabeti mtu wake wa ukoo	
2 K.W.K.	Eneo lenye milima la Yudea	Yohana Mbatizaji azaliwa na kupewa jina; Zekaria atabiri; Yohana ataishi jangwani	
2 K.W.K., karibu Okt. 1	Bethlehemu	Yesu azaliwa; "Neno akawa mwili"	1:1-25
	Karibu na Bethlehemu; Bethlehemu	Malaika awatangazia wachungaji habari njema; malaika wamsifu Mungu; wachungaji wamtembelea mtoto Yesu	
	Bethlehemu; Yerusalemu	Yesu atahiriwa (siku ya 8); wazazi wake wampeleka hekaluni (baada ya siku 40)	
1 K.W.K. au 1 W.K.	Yerusalemu; Bethlehemu; Misri; Nazareti	Wanajimu wamtembelea; familia inakimbilia Misri; Herode awaua wavulana wadogo; familia yarudi kutoka Misri na waishi Nazareti	2:1-23
12 W.K., Pasaka	Yerusalemu	Yesu mwenye umri wa miaka 12 akiwa hekaluni awauliza walimu maswali	
	Nazareti	Arudi Nazareti; aendelea kuwatii wazazi wake; ajifunza useremala; Maria apata watoto wengine wa kiume wanne, na pia watoto wa kike (Mt 13:55, 56; Mk 6:3)	
29 W.K., majira ya kuchipua	Nyikani, Mto Yordani	Yohana Mbatizaji aanza huduma yake	3:1-12

Ramani ya 1

Alama za Ramani

- ⊕ Mwanzo
- Eneo Hususa
- Huenda ni Hapa
- ? Haijulikani kihususa

MARKO	LUKA	YOHANA
	1:5-25	
	1:26-56	
	1:57-80	
	2:1-7	1:14
	2:8-20	
	2:21-38	
	2:39, 40	
	2:41-50	
	2:51, 52	
1:1-8	3:1-18	1:6-8



Mwanzo wa Huduma ya Yesu

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
29, Majira ya kupukutika	Mto Yordani, ng'ambo ya Yordani karibu na au huko Bethania	Yesu abatizwa na kutiwa mafuta; Yehova atangaza kwamba Yesu ni mwanawe na kumkubali	3:13-17
	Nyika ya Yudea	Yesu ajaribiwa na Ibilisi	4:1-11
	Bethania ng'ambo ya Yordani	Yohana Mbatizaji amtambulisha Yesu kuwa Mwana-Kondoo wa Mungu; wanafunzi wa kwanza wajiunga na Yesu	
	Kana ya Galilaya; Kapernaumu	Muujiza wa kwanza kwenye harusi, Yesu ageuza maji kuwa divai; atembelea Kapernaumu	
30, Pasaka	Yerusalemu	Asafisha hekalu	
		Azungumza na Nikodemo	
	Yudea; Ainoni	Yesu atembelea eneo la Yudea, wanafunzi wake wabatiza watu; ushahidi wa mwisho wa Yohana kumhusu Yesu	
	Tiberia; Yudea	Yohana afungwa gerezeni; Yesu aondoka kuelekea Galilaya	4:12; 14:3-5
Sikari, eneo la Samaria	Akiwa njiani kwenda Galilaya, afundisha Wasamaria		




Ramani ya 2

MARKO	LUKA	YOHANA
1:9-11	3:21-38	
1:12, 13	4:1-13	
		1:15, 19-51
		2:1-12
		2:13-25
		3:1-21
		3:22-36
6:17-20	3:19, 20	4:1-3
		4:4-43



Nyika ya Yudea




Huduma Kuu ya Yesu Huko Galilaya


WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
30	Galilaya	Kwanza Yesu atangaza hivi "Ufalme wa mbinguni umekaribia"	4:17
	Kana; Nazareti; Kapernaumu	Amponya mwana wa mtawala; asoma kutoka kwenye kitabu cha Isaya; aenda Kapernaumu	4:13-16
	Bahari ya Galilaya, karibu na Kapernaumu	Awaita wanafunzi wanne: Simoni na Andrea, Yakobo na Yohana	4:18-22
	Kapernaumu	Amponya mama-mkwe wa Simoni na wengine	8:14-17
	Galilaya	Ziara ya kwanza ya Galilaya, na wanafunzi wanne	4:23-25
		Amponya mwenye ukoma; umati wamfuata	8:1-4
	Kapernaumu	Amponya mtu aliyepooza	9:1-8
		Amwita Mathayo; ala pamoja na wakusanya kodi; aulizwa kuhusu kufunga	9:9-17
Yudea	Afundisha kwenye masinagogi		
31, Pasaka	Yerusalemu	Amponya mgonjwa huko Bethzatha; Wayahudi wataka kumuua	
	Arudi kutoka Yerusalemu (?)	Wanafunzi wachuma masuke ya ngano siku ya Sabato; Yesu "Bwana wa Sabato"	12:1-8
	Galilaya; Bahari ya Galilaya	Aponya mkono wa mtu siku ya Sabato; umati wamfuata; aponya watu wengi zaidi	12:9-21
	Mlimani karibu na Kapernaumu	Achagua mitume 12	
	Karibu na Kapernaumu	Mahubiri ya Mlimani	5:1-7:29
	Kapernaumu	Amponya mtumishi wa ofisa wa jeshi	8:5-13
	Naini	Amfufua mwana wa mjane	
	Tiberia; Galilaya (Naini au karibu na hapo)	Yohana awatuma wanafunzi wake kwa Yesu; ukweli wafunuliwa kwa watoto; nira laini	11:2-30
	Galilaya (Naini au karibu na hapo)	Mwanamke mtenda dhambi amimina mafuta kwenye miguu ya Yesu; mfano wa watu wawili wanaodaiwa	
	Galilaya	Safari ya pili ya kuhubiri, akiwa na mitume 12	
		Afukuza roho waovu; dhambi isiyosameheka	12:22-37
		Hatoi ishara yoyote isipokuwa ishara ya Yona	12:38-45
		Mama yake na ndugu zake waja; asema wanafunzi wake ndio ndugu na dada zake	12:46-50

Ramani ya 3A

MARKO	LUKA	YOHANA
1:14, 15	4:14, 15	4:44, 45
	4:16-31	4:46-54
1:16-20	5:1-11	
1:21-34	4:31-41	
1:35-39	4:42, 43	
1:40-45	5:12-16	
2:1-12	5:17-26	
2:13-22	5:27-39	
	4:44	
		5:1-47
2:23-28	6:1-5	
3:1-12	6:6-11	
3:13-19	6:12-16	
	6:17-49	
	7:1-10	
	7:11-17	
	7:18-35	
	7:36-50	
	8:1-3	
3:19-30		
3:31-35	8:19-21	





WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
31 au 32	Eneo la Kapernaumu	Yesu asimulia mifano kuhusu Ufalme	13:1-53
	Bahari ya Galilaya	Atuliza bahari akiwa ndani ya mashua	8:18, 23-27
	Eneo la Gadara	Awatuma roho waovu ndani ya nguruwe	8:28-34
	Huenda ni Kapernaumu	Amponya mwanamke mwenye mtiririko wa damu; amfufua binti ya Yairo	9:18-26
	Kapernaumu (?)	Awaponya vipofu na mabubu	9:27-34
	Nazareti	Akataliwa tena katika mji wa nyumbani kwao	13:54-58
	Galilaya	Safari ya tatu kwenda Galilaya; apanua kazi kwa kuwatuma mitume	9:35-11:1
	Tiberia	Herode amkata kichwa Yohana Mbatizaji; Herode ahangazwa na Yesu	14:1-12
32, karibu na Pasaka (Yoh 6:4)	Kapernaumu (?); Kask. Mash. ya Bahari ya Galilaya	Mitume warudi kutoka safari ya kuhubiri; Yesu alisha wanaume 5,000	14:13-21
	Kask. Mash. ya Bahari ya Galilaya; Genesareti	Wajaribu kumfanya Yesu mfalme; atembea juu ya bahari; aponya wengi	14:22-36
	Kapernaumu	Asema yeye ndiye "mkate wa uzima"; wengi wakwazika na kumwacha	
32, baada ya Pasaka	Labda Kapernaumu	Afunua mapokeo ya wanadamu	15:1-20
	Foinike; Dekapoli	Amponya binti ya mwanamke Msirofoinike; alisha wanaume 4,000	15:21-38
	Magadani	Akataa kutoa ishara ila ya Yona	15:39-16:4



MARKO	LUKA	YOHANA
4:1-34	8:4-18	
4:35-41	8:22-25	
5:1-20	8:26-39	
5:21-43	8:40-56	
6:1-5		
6:6-13	9:1-6	
6:14-29	9:7-9	
6:30-44	9:10-17	6:1-13
6:45-56		6:14-21
		6:22-71
7:1-23		7:1
7:24-8:9		
8:10-12		

Ramani ya 3B



Matukio Karibu na Bahari ya Galilaya

(Pia inaitwa Ziwa la Genesareti au Bahari ya Tiberia)

- 1 Atuliza dhoruba akiwa ndani ya mashua
- 2 Awatuma roho waovu ndani ya nguruwe
- 3 Alisha wanaume 5,000
- 4 Atembea juu ya bahari
- 5 Alisha wanaume 4,000
- 6 Eneo linaloaminiwa kwamba Yesu alitoa Mahubiri ya Mlimani

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
32, baada ya Pasaka	Bahari ya Galilaya; Bethsaida	Akiwa mashuani kuelekea Bethsaida, Yesu aonya kuhusu chachu ya Mafarisayo; amponya mwanamume kipofu	16:5-12
	Eneo la Kaisaria Filipi	Funguo za Ufalme; atabiri kifo na ufufuo wake	16:13-28
	Inaelekea ni Mt. Hermoni	Kugeuka-sura; Yehova azungumza	17:1-13
	Eneo la Kaisaria Filipi	Amponya mvulana aliyekuwa na roho mwovu	17:14-20
	Galilaya	Atabiri tena kuhusu kifo chake	17:22, 23
	Kapernaumu	Alipa kodi kwa sarafu aliyoitoa kwenye kinywa cha samaki	17:24-27
		Mkuu katika Ufalme; mifano: kondoo aliyepotea na mtumwa asiyesamehe	18:1-35
Galilaya-Samaria	Wakielekea Yerusalemu, awaambia wanafunzi wake wadhabihu mambo yote kwa ajili ya Ufalme	8:19-22	


Huduma ya Yesu ya Baadaye Huko Yudea

32, Sherehe ya Vibanda	Yerusalemu	Afundisha kwenye Sherehe; maofisa watumwa ili kumkamata	
		Asema: "Mimi ndiye nuru ya ulimwengu"; amponya mtu aliyezaliwa kipofu	
	Inaelekea ni Yudea	Awatuma wale 70; warudi wakishangilia	
	Yudea; Bethania	Mfano wa Msamaria mwema; Awatembelea Maria na Martha nyumbani	
	Huenda ni Yudea	Afundisha tena ile sala ya kielelezo; mfano wa rafiki aliyeendelea kuomba	
Afukuza roho waovu kwa kutumia nguvu za Mungu; atoa tena ishara ya Yona			
Ala pamoja na Farisayo; ashutumu unafiki wa Mafarisayo			
Mifano: tajiri asiye na akili na msimamizi nyumba mwaminifu			
	Amponya mwanamke kilema siku ya Sabato; mifano ya mbegu ya haradali na chachu		
32, Sherehe ya Wakfu	Yerusalemu	Mchungaji mwema na zizi la kondoo; Wayahudi wajaribu kumpiga mawe; avuka Yordani aenda Bethania	

MARKO	LUKA	YOHANA
8:13-26		
8:27-9:1	9:18-27	
9:2-13	9:28-36	
9:14-29	9:37-43	
9:30-32	9:43-45	
9:33-50	9:46-50	
	9:51-62	7:2-10

		7:11-52
		8:12-9:41
	10:1-24	
	10:25-42	
	11:1-13	
	11:14-36	
	11:37-54	
	12:1-59	
	13:1-21	
		10:1-39

Ramani ya 4 Sidoni




Huduma ya Yesu ya Baadaye Mashariki mwa Yordani

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
32, baada ya Sherehe ya Wakfu	Bethania ng'ambo ya Yordani	Aenda mahali Yohana alipokuwa akibatizia watu; wengi wamwamini Yesu	
	Perea	Afundisha katika miji na vijiji, akisafiri kwenda Yerusalemu	
		Atoa himizo la kuingia kupitia lango jembamba; aombolezea Yerusalemu	
	Huenda ni Perea	Afundisha kuhusu unyenyekevu; mifano ya mahali penye kuonekana zaidi na wageni waliotoa udhuru	
		Hesabu gharama ya kuwa mwanafunzi	
		Mifano ya kondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea, mwana mpotevu	
		Mifano ya msimamizi asiye mwadilifu, tajiri na Lazaro	
		Afundisha kuhusu kukwaza, kusamehe, na imani	
	Bethania	Lazaro afa na kufufuliwa	
	Yerusalemu; Efraimu	Njama ya kumuua Yesu; aondoka	
	Samaria; Galilaya	Awaponya watu kumi wenye ukoma; aeleza jinsi Ufalme wa Mungu utakavyokuja	
	Samaria au Galilaya	Mifano ya mjane aliyeeendelea kuomba, Farisayo na mkusanya-kodi	
	Perea	Afundisha kuhusu ndoa na talaka	19:1-12
		Awabariki watoto	19:13-15
		Swali la tajiri; mfano wa wafanyakazi katika shamba la mizabibu na kiwango kilekile cha mshahara	19:16-20:16
Inaelekea ni Perea	Atabiri kuhusu kifo chake mara ya tatu	20:17-19	
	Ombi la Yakobo na Yohana kupata cheo katika Ufalme	20:20-28	
Yeriko	Apitia huko, awaponya wanaume wawili vipofu; amtembelea Zakayo; mfano wa mina kumi	20:29-34	

Ramani ya 5

MARKO	LUKA	YOHANA
		10:40-42
	13:22	
	13:23-35	
	14:1-24	
	14:25-35	
	15:1-32	
	16:1-31	
	17:1-10	
		11:1-46
		11:47-54
	17:11-37	
	18:1-14	
10:1-12		
10:13-16	18:15-17	
10:17-31	18:18-30	
10:32-34	18:31-34	
10:35-45		
10:46-52	18:35-19:28	




Huduma ya Mwisho ya Yesu Kule Yerusalemu

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
33, Nisani 8	Bethania	Yesu awasili siku sita kabla ya Pasaka	
Nisani 9	Bethania	Maria ammiminia Yesu mafuta kichwani na miguuni	26:6-13
	Bethania-Bethfage-Yerusalemu	Aingia Yerusalemu kwa ushindi, akiwa juu ya punda	21:1-11, 14-17
Nisani 10	Bethania-Yerusalemu	Aulaani mtini; alisafisha hekalu tena	21:18, 19; 21:12, 13
	Yerusalemu	Makuhani wakuu na waandishi wapanga njama ya kumuua Yesu Yehova azungumza; Yesu atabiri kifo chake; kutoamini kwa Wayahudi kwatimiza unabii wa Isaya	
Nisani 11	Bethania-Yerusalemu	Somo la mtini ulionyauka	21:19-22
	Yerusalemu, hekalu	Mamlaka yake yatiliwa shaka; mfano wa wana wawili	21:23-32
		Mifano ya wakulima wauaji wa shamba la mizabibu, karamu ya ndoa	21:33-22:14
		Ajibu maswali kumhusu Mungu na Kaisari, ufufuo, sheria iliyo kuu zaidi	22:15-40
		Aauliza umati ikiwa Kristo ni mwana wa Daudi	22:41-46
		Ole kwa waandishi na Mafarisayo	23:1-39
	Aona mchango wa mjane		
Mlima wa Mizeituni	Ataja ishara ya kuwapo kwake wakati ujao	24:1-51	
	Mifano ya mabikira kumi, talanta, kondoo na mbuzi	25:1-46	
Nisani 12	Yerusalemu	Viongozi Wayahudi wapanga njama ya kumuua	26:1-5
		Yuda apanga jinsi atakavyomsaliti	26:14-16
Nisani 13 (Alhamisi alasiri)	Akiwa Yerusalemu na maeneo ya karibu	Matayarisho ya Pasaka ya mwisho	26:17-19
Nisani 14	Yerusalemu	Ala Pasaka pamoja na mitume wake	26:20, 21
		Awaosha mitume wake miguu	

Ramani ya 6

MARKO	LUKA	YOHANA
		11:55-12:1
14:3-9		12:2-11
11:1-11	19:29-44	12:12-19
11:12-17	19:45, 46	
11:18, 19	19:47, 48	
		12:20-50
11:20-25		
11:27-33	20:1-8	
12:1-12	20:9-19	
12:13-34	20:20-40	
12:35-37	20:41-44	
12:38-40	20:45-47	
12:41-44	21:1-4	
13:1-37	21:5-38	
14:1, 2	22:1, 2	
14:10, 11	22:3-6	
14:12-16	22:7-13	
14:17, 18	22:14-18	
		13:1-20



WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO
Nisani 14	Yerusalemu	Yesu amtaja Yuda kuwa msaliti kisha amfukuza	26:21-25
		Aanzisha Mlo wa Jioni wa Bwana (1Ko 11:23-25)	26:26-29
		Atabiri kwamba Petro atamkana na mitume watatawanyika	26:31-35
		Aahidi kumtuma msaidizi; mfano wa mzabibu wa kweli; atoa amri ya kupendana; sala ya mwisho pamoja na mitume wake	
	Gethsemane	Maumivu makali kwenye bustani; Yesu asalitiwa na kukamatwa	26:30, 36-56
	Yerusalemu	Ahojiwa na Anasi; ahojiwa na Kayafa, Sanhedrini; Petro amkana	26:57-27:1
		Yuda msaliti ajinyonga (Mdo 1:18, 19)	27:3-10
		Mbele ya Pilato, kisha Herode, na kurudi kwa Pilato	27:2, 11-14
Pilato ataka kumwachilia lakini Wayahudi wasema wanamtaka Baraba; ahukumiwa kuuawa kwenye mti wa mateso		27:15-30	
(Karibu saa 9:00 alasiri, Ijumaa)	Golgotha	Afa kwenye mti wa mateso	27:31-56
	Yerusalemu	Mwili wake watolewa mtini na kuwekwa kaburini	27:57-61
Nisani 15	Yerusalemu	Makuhani na Mafarisayo waweka walinzi kulilinda kaburi na kulitia muhuri	27:62-66
Nisani 16	Yerusalemu na maeneo ya karibu; Emau	Yesu afufuliwa; awatokea wanafunzi mara tano	28:1-15
Baada ya Nisani 16	Yerusalemu; Galilaya	Awatokea wanafunzi wake tena na tena (1Ko 15:5-7; Mdo 1:3-8); awafundisha; awatuma kufanya wanafunzi	28:16-20
Iyari 25	Mlima wa Mizeituni, karibu na Bethania	Yesu apaa mbinguni, siku 40 baada ya kufufuliwa (Mdo 1:9-12)	

	MARKO	LUKA	YOHANA
	14:18-21	22:21-23	13:21-30
	14:22-25	22:19, 20, 24-30	
	14:27-31	22:31-38	13:31-38
			14:1- 17:26
	14:26, 32-52	22:39-53	18:1-12
	14:53-15:1	22:54-71	18:13-27
	15:1-5	23:1-12	18:28-38
	15:6-19	23:13-25	18:39- 19:16
	15:20-41	23:26-49	19:16-30
	15:42-47	23:50-56	19:31-42
	16:1-8	24:1-49	20:1-25
			20:26- 21:25
		24:50-53	



Nyongeza A

Kanuni za Kutafsiri Biblia	A1
Sehemu za Toleo Hili	A2
Jinsi Biblia Ilivyotufikia	A3
Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kiebrania	A4
Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo	A5
Chati: Manabii na Wafalme wa Yuda na Israeli	A6
Matukio Muhimu Katika Maisha ya Yesu Duniani	A7

Mwanzoni Biblia iliandikwa katika Kiebrania, Kiaramu, na Kigiriki cha kale. Leo inapatikana ikiwa nzi-ma au kwa sehemu katika lugha 3,000 hivi. Idadi kubwa ya watu wanaosoma Biblia hawaelewi lugha za awali na hivyo lazima wategeme tafsiri. Ni kanuni gani zinapaswa kufuatwa katika kutafsiri Biblia, na zilitumiwaje katika kutafsiri *Biblia Takatifu* —*Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*?

Huenda wengine wakafikiri kwamba tafsiri ya neno kwa neno inaweza kuwasaidia wasomaji wapate maana inayokaribiana zaidi na ile iliyo katika lugha za awali. Hata hivyo, si lazima iwe hivyo. Fikiria baadhi ya sababu:

- Hakuna lugha mbili zinazofanana kabisa katika sarufi, msamiati, na muundo wa sentensi. Profesa wa Kiebrania, S. R. Driver, aliandika kwamba lugha “hazitofautiani tu katika sarufi na mizizi, bali pia . . . jinsi ambavyo mawazo yanaunganishwa katika sentensi.” Lugha tofauti hutumia njia tofauti za kufikiri. “Kwa hiyo,” anaendelea kusema Profesa Driver, “miundo ya sentensi katika lugha mbalimbali hutofautiana.”
- Hakuna lugha yoyote ya kisasa inayofanana kabisa na msamiati na sarufi ya Kiebrania, Kiaramu, na Kigiriki kilichotumiwa kuandika Biblia, kwa hiyo, huenda tafsiri ya neno kwa neno ya Biblia isieleweke au hata nyakati nyingine ikapotosha maana.
- Maana ya neno au maneno inaweza kubadilika ikitegemea muktadha.

Katika baadhi ya sehemu, mtafsiri anaweza kutafsiri lugha ya awali neno na kwa neno kwa usahihi, lakini anapaswa kuwa makini sana.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano inayoonyesha jinsi tafsiri ya neno kwa neno inavyoweza kueleweka vibaya:

- Maandiko hutumia maneno ‘kulala usingizi’ kumaa-nisha usingizi halisi na usingizi wa kifo. (Mathayo 28:13; Matendo 7:60) Maneno hayo yanapotumiwa kwenye muktadha

unaorejezea kifo, watafsiri wa Biblia wanaweza kutumia maneno kama ‘kulala usingizi katika kifo,’ ambayo humsaidia msojaji wa kisasa aelewe maana.—1 Wakorintho 7:39; 1 Wathesalonike 4:13; 2 Petro 3:4.

- Mtume Paulo alitumia maneno yanayopatikana katika Waefeso 4:14 ambayo yanaweza kutafsiriwa neno kwa neno kuwa “katika mchezo wa dadu wa wanaume.” Msembo huo wa kale unarejezea zoea la kuwadanganya watu kwa kutumia dadu. Katika lugha nyingi, tafsiri ya neno kwa neno ya msembo huo haieleweki vizuri. Kutafsiri msembo huo kuwa “udanganyifu wa watu” ni njia iliyo wazi zaidi ya kutokeza maana.
- Andiko la Waroma 12:11 linatumia msembo wa Kigiriki ambao ukitafsiriwa neno na kwa neno unamaanisha “katika kuchemka kwa roho.” Katika Kiswahili, maneno hayo hayatokezi maana iliyokusudiwa, kwa hiyo katika tafsiri hii yametafsiriwa kuwa ‘kuwaka roho.’
- Katika mahubiri yake maarufu ya mlimani, Yesu alitumia maneno ambayo mara nyingi hutafsiriwa kuwa “Heri walio maskini wa roho.” (Mathayo 5:3, *Union Version*) Lakini katika lugha nyingi, tafsiri ya neno kwa neno ya mstari huo haieleweki. Katika visa fulani, tafsiri ya neno kwa neno inaweza kumaanisha kwamba “maskini wa roho” ni watu walio na matatizo ya kiakili au walio dhaifu na wasio na msimamo. Hata hivyo, hapa Yesu alikuwa akiwafundisha watu kwamba furaha yao haikutegemea kutosheleza mahitaji yao ya kimwili, bali kutambua kwamba wanahitaji mwongozo wa Mungu. (Luka 6:20) Kwa hiyo, maneno kama vile “wale wanaotambua uhitaji wao wa kiroho” au “wale wanaotambua kwamba wanahitaji Mungu” hutokeza kwa usahihi maana ya maneno ya awali.—Mathayo 5:3; *The New Testament in Modern English*.
- Katika muktadha mbalimbali, neno la Kiebrania linalotafsiriwa kuwa “wivu” linalingana na maana ya neno la Kiswahili, yaani, kukasirika kwa sababu rafiki wa karibu amekosa uaminifu au kuwaonea wivu watu kwa sababu ya mali zao. (Methali 6:34; Isaya 11:13) Hata hivyo, neno hilohilo la Kiebrania lina maana nzuri. Kwa mfano, linaweza kutumiwa kumaanisha “bidii,” au ulinzi ambao Yehova anawapa watumishi wake au jinsi

ΟΙΠΤΩΧΟΙ
ΤΩΠΝΕΥΜΑΤΙ

MATHAYO 5:3

Tafsiri ya neno
kwa neno: “maskini
wa roho”

Wazo: “wale
wanaotambua
uhitaji wao wa
kiroho”

anavyotaka ‘wamwabudu yeye peke yake.’ (Kutoka 34:14; 2 Wafalme 19:31; Ezekieli 5:13; Zekaria 8:2) Pia linaweza kutumiwa kumaanisha “bidii” ya watumishi wake waaminifu kwa ajili ya Mungu na ibada yake au jinsi ambavyo ‘hawavumilii ushindani wowote’ kumwelekea.—Zaburi 69:9; 119:139; Hesabu 25:11.

- Neno la Kiebrania ambalo mara nyingi hurejelea mkono wa mwanadamu lina maana mbalimbali. Ikitegemea muktadha neno hilo linaweza kutafsiriwa kuwa “mamlaka,” “ukarimu,” au “nguvu.” (2 Samweli 8:3; 1 Wafalme 10:13; Methali 18:21) Kwa kweli, neno hilo limetafsiriwa kwa zaidi ya njia 40 tofauti-tofauti katika toleo la Kiingereza la *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

ገ

Neno la Kiebrania *yadh* kwa kawaida hutafsiriwa kuwa “mkono,” lakini ikitegemea muktadha, neno hili linaweza kutafsiriwa kuwa “mamlaka,” “ukarimu,” “nguvu,” na kwa njia nyingine nyingi

Kutokana na sababu hizo, kutafsiri Biblia kunahusisha mengi zaidi ya kutafsiri neno la lugha ya awali kwa kutumia neno lililele kila mara. Mtafsiri anapaswa kutumia busara ili kuchagua maneno ambayo yanawakilisha vizuri mawazo ya maandishi ya lugha ya awali. Isitoshe, anapaswa kupanga sentensi katika njia inayofuata sheria za sarufi za lugha inayolengwa, na hivyo kufanya maandishi yasomeke kwa urahisi.

Wakati huohuo mtafsiri hapaswi kupita mipaka anapotumia maneno tofauti ili kueleza maandishi. Mtafsiri ambaye bila kujali anafafanua ujumbe wa Biblia kulingana na jinsi anavyoelewa wazo kuu anaweza kupotosha maana ya maandishi. Jinsi gani? Mtafsiri anaweza kuingiza kimakosa maoni

yake kuhusu maana ya maandishi ya awali au huenda akaondoa habari muhimu zilizoko kwenye maandishi ya awali. Kwa hiyo, ingawa huenda tafsiri za Biblia zilizofafanuliwa zikasomeka kwa urahisi, nyakati nyingine huenda uhuru huo ukafanya wasomaji wasipate ujumbe halisi wa maandishi.

Ni rahisi kwa mtafsiri kuathiriwa na msimamo wa kidini. Kwa mfano, andiko la Mathayo 7:13 linasema “Barabara inayoongoza kwenye uharibifu ina nafasi kubwa.” Baadhi ya watafsiri ambao labda wameathiriwa na msimamo wa kidini, wametumia maneno “moto wa mateso” badala ya maana halisi ya neno la Kigiriki, yaani, “uharibifu.”

Pia, mtafsiri anapaswa kukumbuka kwamba Biblia iliandikwa kwa kutumia lugha iliyotumiwa na watu wa kawaida, kama vile waku-lima, wachungaji, na wavuvi. (Nehemia 8:8, 12; Matendo 4:13)

Kwa hiyo, tafsiri nzuri ya Biblia hufanya ujumbe wake ueleweke kwa watu wanyoofu, wa malezi mbalimbali. Maneno yaliyo wazi, ya kawaida, na yanayoeleweka kwa urahisi yanafaa kuliko maneno ambayo hayatumwi sana na watu wa kawaida.

Idadi kubwa ya watafsiri wa Biblia wamefanya uamuzi usio na misingi wa kuondoa jina la Mungu, Yehova, kutoka katika tafsiri za kisasa ingawa jina hilo linapatikana katika hati za kale za Biblia. (Angalia Nyongeza A4.) Tafsiri nyingi huondoa jina hilo na kutumia jina la cheo, kama vile “Bwana,” na nyingine hata huficha ukweli wa kwamba Mungu ana jina. Kwa mfano, katika baadhi ya tafsiri, sala ya Yesu kwenye Yohana 17:26 inasema: “Nimekufanya ujulikane kwao,” na kwenye Yohana 17:6, “Nimekufunua kwa wale ulionipa.” Hata hivyo, tafsiri sahihi ya sala ya Yesu inasema: “Nimewajulisha *jina lako*,” na “Nimelifunua *jina lako* kwa watu ulionipa.”

Kama ilivyotajwa katika utangulizi wa toleo la kwanza la Kiingereza la *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*: “Hatufafanui Maandiko. Tumejitahidi kutafsiri neno kwa neno inapowezekana, mahali ambapo misemo ya Kiingereza ya kisasa inaruhusu na mahali ambapo tafsiri ya neno kwa neno haifichi maana.” Kwa hiyo, Halmashauri ya Biblia ya Tafsiri ya Ulimwengu Mpya imejitahidi kusawazisha kati ya kutumia maneno na misemo inayofanana na ile iliyo kwenye hati za kale, na wakati huohuo, kuepuka maneno ambayo hayaeleweki au yanayoficha mawazo yaliyokusudiwa. Matokeo ni kwamba Biblia inaweza kusomeka kwa urahisi na msomaji anaweza kuwa na uhakika kabisa kwamba ujumbe wa Biblia ulioongozwa na roho ya Mungu umetafsiriwa kwa usahihi.—1 Wathesalonike 2:13.

Tafsiri inayotegemeka inapaswa:

- Kulitakasa jina la Mungu kwa kulirudisha mahali pake panapofaa katika Maandiko.—Mathayo 6:9.
- Kuwasilisha kwa usahihi ujumbe wa awali ulioongozwa na roho ya Mungu.—2 Timotheo 3:16.
- Kutafsiri neno kwa neno ikiwa maneno na muundo wa lugha inayolengwa unaruhusu kutafsiri maandishi ya awali kwa njia hiyo.
- Kuwasilisha kwa usahihi maana ya neno au maneno ikiwa tafsiri ya neno kwa neno inaweza kupotosha au kuficha maana.
- Kutumia lugha ya kawaida, inayoeleweka kwa urahisi na iliyo rahisi kusoma.—Nehemia 8:8, 12.

Tafsiri ya Ulimwengu Mpya ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo ilitolewa katika Kiingereza mwaka wa 1950, na toleo zima la *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* lilichapishwa mwaka wa 1961. Tangu wakati huo makumi ya mamilioni ya wasomaji katika lugha zaidi ya 180 wamefaidika na tafsiri hii sahihi na inayosomeka ya Maandiko Matakatifu iliyotafsiriwa kutoka kwa lugha za awali.

Halmashauri ya sasa ya Biblia ya Tafsiri ya Ulimwengu Mpya inatambua uhitaji wa kutumia lugha inayogusa mioyo ya wasomaji wa kisasa. Kwa sababu hiyo, kanuni kadhaa za muundo na msamiati zilifuatwa katika tafsiri hii ili kutimiza mambo yafuatayo:

- **Kutumia lugha ya kisasa na inayoeleweka.** Kwa mfano, neno “ustahimilivu” linaweza kueleweka kimakosa kumaanisha “mtu anayeteseka kwa muda mrefu.” Hata hivyo, wazo linalokusudiwa ni kujizuia kwa hiari, ambalo linatokezwa vizuri zaidi kwa kutumia neno “subira.” (Wagalatia 5:22) Katika toleo hili, maneno “karamu za kupindukia” yametafsiriwa kuwa “karamu zenye vurugu.” (Wagalatia 5:19-21) Maneno “wakati usio na kipimo” yaliondolewa na badala yake maneno kama vile “milele,” “kudumu,” “zamani za kale” yakatumia ili kutokeza maana iliyokusudiwa katika kila muktadha.—Mwanzo 3:22; Kutoka 31:16; Zaburi 90:2; Mhubiri 1:4; Mika 5:2.

Katika Kiebrania na Kigiriki cha kale neno “mbegu” linaweza kumaanisha mbegu ya mmea na pia uzao wa wanadamu, au wazao, au shahawa. Kwa kuwa si kawaida katika lugha ya Kiswahili kutumia neno “mbegu” kurejelea wanadamu, neno hilo liliondolewa na badala yake maneno yanayotokeza maana inayokusudiwa yakatumia walingana na muktadha. (Mwanzo 1:11; 22:17; 48:4; Mathayo 22:24; Yohana 8:37) Mara nyingi, neno “uzao” sasa linatumia kurejelea ahadi iliyotolewa katika Edeni, kwenye Mwanzo 3:15.

- **Maneno yaliyo katika Biblia yafafanuliwa.** Katika matoleo yaliyotangulia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* ya Kiingereza, neno la Kiebrania *ne'phesh* na neno la Kigiriki *psy-khe'* kila mara yalitafsiriwa kuwa “nafsi.” Kwa sababu ya maoni mengi

yasiyo ya kweli kuhusu maana ya neno “nafsi,” mbinu hiyo ilimsaidia msomaji kuelewa jinsi waandikaji wa Biblia walioongozwa na roho ya Mungu walivyotumia maneno hayo ya lugha ya awali. Ikitegemea muktadha, maneno hayo yanaweza kumaanisha (1) mtu, (2) uhai wa mwanadamu, (3) viumbe walio hai, (4) tamaa na hamu ya mtu au, mara nyingine, (5) hata watu waliokufa. Hata hivyo, kwa kuwa matumizi kama hayo ya neno “nafsi” si ya kawaida katika Kiswahili, uamuzi ulifanywa ili kutafsiri maneno hayo ya lugha ya awali kulingana na maana iliyokusudiwa, mara nyingi yakiwa na maelezo ya chini yanayosema “Au ‘nafsi.’” (Kwa mfano, angalia, Mwanzo 1:20; 2:7; Mambo ya Walawi 19:28; Zaburi 3:2; Methali 16:26; Mathayo 6:25.) Hata hivyo, katika mashairi na mistari inayojulikana, neno “nafsi” limedumishwa, pamoja na maelezo ya chini yanayoelekeza kwenye Kamusi au yanayoonyesha maana nyingine.—Kumbukumbu la Torati 6:5; Zaburi 131:2; Methali 2:10; Mathayo 22:37.

Vivyo hivyo, neno figo lilidumishwa linaporejelea kiungo halisi. Hata hivyo, linapotumiwa kwa njia ya mfano kama vile kwenye Zaburi 7:9 na 26:2 na Ufunuo 2:23, wazo lililokusudiwa la “hisia za ndani kabisa” au “mawazo ya ndani kabisa” limeandikwa kwenye mistari, na tafsiri ya neno kwa neno kwenye maelezo ya chini.

Kama ilivyo katika Kiebrania na Kigiriki, neno la Kiswahili “moyo” lina maana halisi na maana ya mfano, basi mara nyingi lilidumishwa katika mistari. Hata hivyo, katika sehemu chache ambapo maana haikueleweka, ujumbe ulitafsiriwa kwa njia iliyo wazi zaidi. Kwa mfano, katika kitabu cha Methali, maneno “aliyepungukiwa moyoni” sasa yametafsiriwa kuwa “asiye na busara,” nayo tafsiri ya neno kwa neno imewekwa kwenye maelezo ya chini. (Methali 6:32; 7:7) Maneno mengine, kama vile, “unono,” “mwili,” na “pembe,” yalishughulikiwa kwa njia hiyo, kulingana na muktadha. (Mwanzo 45:18; Mhubiri 5:6; Ayubu 16:15) Baadhi ya maneno hayo yanafafanuliwa katika “Kamusi ya Maneno ya Biblia.”

- **Kusomeka kwa urahisi.** Katika matoleo yaliyotangulia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*, vitenzi visaidizi vilitumiwa kuonyesha ikiwa kitenzi cha Kiebrania kilikuwa kimekamilika au la. Kwa mfano, kitendo kinachoendelea ambacho mara nyingi huelezwa kwa kutumia kitenzi ambacho hakikamilikana, kilionyesha kwa kutumia maneno kama “akaendelea,” “ikawa,” na kadhalika. Mkazo ambao mara nyingi huwasilishwa na kitenzi cha Kiebrania kilichokamilika ulionyesha

kwa kuongezea maneno “kwa hakika,” “lazima,” na maneno kama hayo. Kwa hiyo, maneno hayo yalitumiwa mara nyingi sana katika maandishi. Katika toleo hili, vitenzi visaidizi vilidumishwa katika sehemu fulani kwa kutumia maneno kama vile “kuendelea,” na “alizoza” kulipokuwa na sababu za msingi za kuonyesha kitendo kinachoendelea. (Mwanzo 3:9; 34:1; Methali 2:4) Hata hivyo, yaliondolewa ili kurahisisha usomaji wakati vitenzi visaidizi havikuhitajiwa katika kuwasilisha maana iliyokusudiwa mwanzoni.

- **Kuwasilisha mawazo sahihi ya maneno yanayohusu jinsia.** Maneno ya Kiebrania na Kigiriki huonyesha jinsia ya kiume au ya kike, na katika Kigiriki, pia kuna maneno yasiyo na jinsia. Hata hivyo, nyakati nyingine, kuonyesha jinsia ya maneno ya lugha ya awali kunaweza kuficha maana iliyokusudiwa. Katika Kiebrania na Kigiriki, maneno yaliyo katika wingi kwa kawaida huwa na jinsia ya kiume, si yanaporejelea wanaume tu bali pia yanaporejelea wanaume na wanawake. Kwa mfano, ingawa maneno “wana wa Israeli” yanaweza kurejelea wana 12 wa Yakobo, mara nyingi hurejelea taifa zima la Israeli, wanaume na wanawake. (Mwanzo 46:5; Kutoka 35:29) Kwa hiyo, katika toleo hili, mara nyingi maneno hayo yanatafsiriwa kuwa “Waisraeli” ili kuonyesha kwamba inarejelea taifa zima. Vivyo hivyo, maneno “mvulana asiye na baba” yametafsiriwa kuwa “mtoto asiye na baba” au “yatima” ili kuonyesha kwamba yanaweza kurejelea mvulana au msichana. Kwa upande mwingine, kwa kuwa Biblia inatumia jinsia ya kiume inaporemjelea Mungu na Mwana wake, na pia malaika mbalimbali na roho waovu, hakuna msingi wa kutumia maneno yasiyo na jinsia kama inavyofanywa katika baadhi ya tafsiri za kisasa.

Marekebisho yote katika maandishi ya Biblia yalifanywa kwa sala, kwa makini, na kwa heshima kubwa kuelekea kazi nzuri iliyofanywa mwanzoni na Halmashauri ya Biblia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

Sehemu nyingine za toleo hili:

Toleo hili la Biblia lina maelezo ya chini. Kwa ujumla kuna aina zifuatazo za maelezo ya chini:

“Au”

Njia mbalimbali ambazo maandishi ya Kiebrania, Kiaramu, au Kigiriki yanaweza kutafsiriwa ili kutokeza wazo lililile.—Mwanzo 1:2, maelezo ya chini kwenye neno “nguvu ya utendaji ya Mungu”; Yohana 1:8, “sauti ya chini.”

“Au labda”	Njia nyingine ambazo maandishi yanaweza kutafsiriwa na kuwasilisha wazo linalokubalika lakini lililo tofauti.—Mwanzo 21:6, “atacheka pamoja nami”; Zekaria 14:21, “Mkanaani.”
“Tnn.”	Tafsiri ya neno kwa neno ya Kiebrania, Kiaramu, au Kigiriki au maana ya msingi ya maneno ya lugha ya awali.—Mwanzo 30:22, “mimba”; Kutoka 32:9, “wakaidi.”
Maana na maelezo ya ziada	Maana ya majina (Mwanzo 3:17, “Adamu”; Kutoka 15:23, “Mara”); habari kuhusu uzito na vipimo (Mwanzo 6:15, “mikono”); habari muhimu kwenye Nyongeza na Kamusi.—Mwanzo 37:35, “Kaburini”; Mathayo 5:22, “Gehena.”

Sehemu iliyo upande wa mbele, yenye kichwa “Utangulizi wa Neno la Mungu,” ina muhtasari wa mafundisho ya msingi yanayopatikana kwenye Biblia. Baada ya kitabu cha Ufunuo kuna “Orodha ya Vitabu vya Biblia,” “Fahirisi,” na “Kamusi ya Maneno ya Biblia.” Kamusi hiyo humsaidia msomaji aelewe maneno yaliyoorodheshwa humo kulingana na matumizi yake hususa katika Biblia. Nyongeza A ina sehemu zifuatazo “Kanuni za Kutafsiri Biblia,” “Sehemu za Toleo Hili,” “Jinsi Biblia Ilivyotufikia,” “Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kiebrania,” “Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo,” “Chati: Manabii na Wafalme wa Yuda na Israeli,” na “Matukio Muhimu Katika Maisha ya Yesu Duniani.” Nyongeza B ina ramani, chati, na habari nyingine muhimu kwa wanafunzi wenye bidii wa Biblia.

Kila kitabu cha Biblia kina sehemu ya yaliyomo, ambayo ina habari zilizo katika sura za kitabu hicho, pamoja na mistari hususa, na hivyo kumpa msomaji muhtasari wa kitabu chote. Sehemu ya katikati kwenye kila ukurasa ina marejeo muhimu zaidi kutoka katika matoleo yaliyotangulia, yanayoonyesha mistari ya Biblia inayohusiana.

Mtungaji na Mwanzilishi wa Biblia ndiye aliyehifadhi pia. Yeye ndiye aliyefanya maneno haya yaa-ndikwe:

“Neno la Mungu wetu hudumu milele.”

—Isaya 40:8.

Maneno hayo ni ya kweli hata ingawa hakuna hati ya Biblia ya awali ya Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu* au Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo iliyopo leo. Kwa hiyo, tunawezaje kuwa na uhakika kabisa kwamba ujumbe ulio katika Biblia leo kwa kweli ndio uliokuwa katika maandishi ya awali yaliyoongozwa na roho ya Mungu?

WANAKILI WALILIHIFADHI NENO LA MUNGU

Kuhusu Maandiko ya Kiebrania, iliwezekana kwa sababu ya desturi ya kale iliyoanzishwa na Mungu, aliyesema kwamba maandishi yanapaswa kunakiliwa.[#] Kwa mfano, Yehova aliwaagiza wafalme wa Israeli wajiandikie nakala zao za Sheria iliyoandikwa. (Kumbukumbu la Torati 17:18) Pia, Mungu aliwapa Walawi jukumu la kuhifadhi Sheria na kuwafundisha watu kuihusu. (Kumbukumbu la Torati 31:26; Nehemia 8:7) Baada ya Wayahudi kupelekwa utekwani Babiloni, kukawa na kikundi cha wanakili, au maandishi (Wasoferi). (Ezra 7:6, maelezo ya chini) Baada ya muda, maandishi hao walitokeza nakala nyingi za vitabu 39 vya Maandiko ya Kiebrania.

Kwa karne nyingi, maandishi walinakili vitabu hivyo kwa makini. Katika Enzi za Kati, kikundi cha maandishi Wayahudi kilichoitwa Wamasora kiliendeleza desturi hiyo. Hati kamili ya kale zaidi ya Wamasora ni Kodeksi ya Leningrad, ya mwaka 1008/1009 W.K. Hata hivyo, katikati ya karne ya 20, hati 220 za Biblia au visehemu vilipatikana kati ya Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chu-

* Kuanzia hapa yanarejelewa kama Maandiko ya Kiebrania.

[#] Sababu moja iliyofanya hati zinakiliwe ni kwamba hati za awali ziliandikwa kwenye vitu vilivyoharibika haraka.

mvi. Hati hizo za Biblia ziliandikwa zaidi ya miaka 1000 kabla ya Kodeksi ya Leningrad. Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi vinapolinganishwa na Kodeksi ya Leningrad jambo muhimu linathibitika: Ingawa Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi vina tofauti fulani katika maneno, tofauti hizo hazithiri ujumbe wenyewe.

Namna gani kuhusu vile vitabu 27 vya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo? Vitabu hivyo viliandikwa kwanza na baadhi ya mitume wa Yesu Kristo na wanafunzi wa mapema. Kwa kufuata desturi ya waandishi Wayahudi, Wakristo wa mapema walitokeza nakala za vitabu hivyo. (Wakolosai 4:16) Licha ya jitahada za Maliki Mroma Diokletiani na wengine kuharibu maandishi yote ya Wakristo wa mapema, maelfu ya visehemu na hati za kale zimehifadhiwa hadi leo.

Pia, maandishi ya Wakristo yalitafsiriwa katika lugha nyingine. Tafsiri za awali za Biblia zinatia ndani nakala za lugha za kale kama vile Kiarmenia, Kikoptiki, Kiethiopia, Kigeorgia, Kilatini, na Kisiria.

KUCHAGUA MAANDISHI YA KIEBRANIA NA YA KIGIRIKI KWA AJILI YA KUTAFSIRI

Si nakala zote za hati za kale za Biblia zilizo na maneno yanayofanana. Hivyo basi, tuna-wezaje kujua ujumbe uliokuwa katika hati za awali?

Hali hiyo inaweza kulinganishwa na mwalimu anayewaomba wanafunzi 100 wanakili sura fulani ya kitabu. Hata kama baadaye nakala ya awali itapotea, kulinganisha zile nakala 100 bado kunaweza kufunua ujumbe wa maandishi ya awali. Ingawa huenda kila mwanafunzi akafanya makosa, ni vigumu kwa wanafunzi wote kufanya makosa yaleyale. Vivyo hivyo, wasomi wanapolinganisha maelfu ya visehemu na nakala za vitabu vya Biblia vya kale vina-vyopatikana, wanaweza kutambua makosa ya wanakili na kujua maneno yaliyokuwapo awali.

Tunawezaje kuwa na uhakika kwamba mawazo yaliyokuwa katika maandishi ya awali ya Biblia yamewasilishwa kwetu kwa usahihi? Akizungumza kuhusu maandishi ya Maandiko ya Kiebrania, msomi William H. Green alisema hivi: “Inaweza kusemwa kwa uhakika kwamba hakuna maandishi mengine ya kale yaliyowasilishwa kwa usahihi mkubwa hivyo.” Kuhusu Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, ambayo huitwa Agano Jipya, msomi wa Biblia F. F. Bruce aliandika hivi: “Uthibitisho wa maandishi yetu ya Agano Jipya ni

“Inaweza kusemwa kwa uhakika kwamba hakuna maandishi mengine ya kale yaliyowasilishwa kwa usahihi mkubwa hivyo”

Sura ya 40 ya kitabu cha Isaya katika Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi (ya mwaka wa 125 mpaka 100 K.W.K.)

Yanapolinganishwa na hati za Kiebrania zilizoandikwa miaka elfu moja baadaye, kuna tofauti ndogo tu, hasa katika kuandika maneno



Sura ya 40 ya kitabu cha Isaya katika Kodeksi ya Aleppo, hati muhimu ya Kiebrania ya Wamasora ya karibu mwaka wa 930 W.K.



mkubwa zaidi kuliko uthibitisho wa maandishi mengi ya waandikaji wa kale, na hakuna mtu anayeweza kutilia shaka usahihi wake." Pia anasema: "Ikiwa Agano Jipya lingekuwa mkusanyo wa maandishi ya kilimwengu, usahihi wake haungetiliwa shaka kamwe."

Maandishi ya Kiebrania: *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya ya Maandiko ya Kiebrania* katika Kiingereza (1953-1960) ilitegemea *Biblia Hebraica*, ya Rudolf Kittel. Tangu wakati huo, matoleo yaliyoboreshwa ya maandishi ya Kiebrania, yaani, *Biblia Hebraica Stuttgartensia* na *Biblia Hebraica Quinta*, yameongeza utafiti wa karibuni unaotegemea Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi na hati nyingine za kale. Maandishi hayo ya wasomi yanafanana na Kodeksi ya Leningrad na yana maelezo ya chini yaliyo na maneno yenye ulinganifu kutoka vyanzo vingine, kutia ndani Pentateuki ya Samaria, Vitabu vya Kukunjwa vya Bahari ya Chumvi, *Septuaginta* ya Kigiriki, Targumi za Kiaramu, *Vulgate* ya Kilatini, na *Peshitta* ya Kisiria. *Biblia Hebraica Stuttgartensia* na *Biblia Hebraica Quinta* zilitumiwa katika kuandaa toleo hili la *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

Maandishi ya Kigiriki: Mwishoni mwa karne ya 19, msomi B. F. Westcott na F.J.A. Hort walilinganisha hati za Biblia na visehemu vilivyokuwapo walipokuwa wakiandaa maandishi ya Kigiriki ambayo walihisi yalikalibiana zaidi na maandishi ya awali. Katikati ya karne ya 20 Halmashauri ya Biblia ya Tafsiri ya Ulimwengu Mpya ilitumia maandishi hayo kama msingi wa tafsiri yao. Pia, walitumia mafunjo mengine ya kale, yanayodhaniwa kuwa ya karne ya pili au ya tatu W.K. Tangu wakati huo, mafunjo mengi zaidi yamepatikana. Isitoshe, maandishi kama yale ya Nestle na Aland na ya *United Bible Societies* yana utafiti wa karibuni zaidi wa wasomi. Baadhi ya habari zilizo katika utafiti huo zimetumiwa katika toleo hili.


Kwa msingi wa maandishi hayo, ni wazi kwamba baadhi ya mistari katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo iliyokuwa katika tafsiri za zamani, kama vile *King James Version*, kwa kweli ilikuwa imeongezwa na wanakili wa baadaye na haikuwa kamwe sehemu ya Maandiko yaliyoongozwa na roho ya Mungu. Hata hivyo, kwa kuwa kugawanywa kwa mistari ambako kwa kawaida kunakubalika katika tafsiri za Biblia tayari kulikuwa kumeanzishwa katika karne ya 16, kuondolewa kwa mistari hiyo huacha mapengo katika mistari fulani ya Biblia nyingi. Mistari hiyo ni Mathayo 17:21; 18:11; 23:14; Marko 7:16; 9:44, 46; 11:26; 15:28; Luka 17:36; 23:17; Yohana 5:4; Matendo 8:37; 15:34; 24:7; 28:29; na Waroma 16:24. Katika toleo hili lililorekebisha, mistari hiyo iliyoondolewa ina maelezo ya chini mahali inapopatikana.

Kuhusu umalizio mrefu wa Marko 16 (mistari ya 9-20), umalizio mfupi wa Marko 16, na maneno yaliyo kwenye Yohana 7:53-8:11, ni wazi kwamba mistari hiyo haikuwa katika hati za awali. Kwa hiyo, maandishi hayo yaliyoongezwa hayajawekwa kwenye toleo hili.*

Baadhi ya maneno yamerekebishwa ili kutia ndani mawazo ambayo kwa kawaida wasomi huyakubali kuwa mawazo sahihi zaidi ya maandishi ya awali. Kwa mfano, kulingana na baadhi ya hati, andiko la Mathayo 7:13 linasema: “Ingieni kupitia lango jembamba, kwa sababu lango ni pana, na barabara inayoongoza kwenye uharibifu ina nafasi kubwa.” Katika matoleo yaliyotangulia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*, maneno “lango ni” hayakuwapo. Hata hivyo, uchunguzi zaidi wa hati ulithibitisha kwamba maneno “lango ni” yalikuwa katika maandishi ya awali. Basi yalitiwa ndani kwenye toleo hili. Kuna marekebisho mengine kama hayo. Hata hivyo, marekebisho hayo ni madogo, na hayabadili ujumbe wa msingi wa Neno la Mungu.

* Habari zaidi kuhusu kwa nini mistari hiyo inaonwa kuwa ya kuongezwa inaweza kupatikana kwenye maelezo ya chini ya *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*—Yenye Marejezo katika Kiingereza ya mwaka 1984.

Hati ya mafunjo ya
2 Wakorintho 4:13-5:4
ya karibu mwaka wa
200 W.K.



Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kiebrania

Jina la Mungu, linalowakilishwa na konsonanti nne za Kiebrania יהוה, linapatikana karibu mara 7,000 katika Maandiko ya Kiebrania. Katika tafsiri hii herufi hizo nne, zinazojulikana kama Tetragramatoni, zimetafsiriwa kuwa “Yehova.” Hilo ndilo jina linalopatikana mara nyingi zaidi katika Biblia. Ingawa waandikaji walioongozwa na roho takatifu walimtaja Mungu kwa kutumia majina ya cheo, kama vile “Mweza-Yote,” “Aliye Juu Zaidi,” na “Bwana,” walitumia hasa Tetragramatoni kuandika jina binafsi la Mungu.

Yehova Mungu ndiye aliyewaongoza waandikaji wa Biblia kutumia jina lake. Kwa mfano, alimwongoza nabii Yoeli kuandika hivi: “Kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokolewa.” (Yoeli 2:32) Na Mungu alimtumia mtungazaburi mmoja kuandika: “Na watu wajue kwamba wewe, ambaye jina lako ni Yehova, wewe peke yako ndiye Uliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote.” (Zaburi 83:18) Kwa kweli, jina la Mungu linapatikana mara 700 hivi katika kitabu cha Zaburi peke yake—ambacho ni kitabu chenye maandishi ya ushairi yaliyoimbwa na kukaririwa na watu wa Mungu. Basi, kwa nini tafsiri nyingi za Biblia hazina jina la Mungu? Kwa nini tafsiri hii imetumia jina “Yehova”? Na jina la Mungu, Yehova, linamaanisha nini?

Kwa nini jina hilo halipatikani katika tafsiri nyingi za Biblia? Kuna sababu mbalimbali. Watu fulani husema kwamba Mungu Mweza-Yote hapaswi kutambulishwa kwa jina la kipekee. Wengine wanafuata desturi ya Kiyahudi ya kutolitumia jina hilo, labda kwa kuogopa kulikufuru. Nao wengine wanaamini kwamba kwa kuwa hakuna mtu anayejua kikamili jinsi jina la Mungu lilivyotamkwa, ni afadhali kutumia jina la cheo, kama vile “Bwana” au “Mungu.” Hata hivyo, maoni hayo hayana msingi kwa sababu zifuatazo:

- Wale wanaodai kwamba Mungu Mweza-Yote hapaswi kutambulishwa kwa jina la kipekee wanapuza uthibitisho wa kwamba nakala za awali za Neno lake, kutia ndani nakala

יהוה

Jina la Mungu katika herufi za kale za Kiebrania zilizotumiwa kabla ya Wayahudi kwenda utekwani Babiloni

יהוה

Jina la Mungu katika herufi za Kiebrania zilizotumiwa baada ya Wayahudi kutoka utekwani Babiloni

Handwritten text in a cursive script, likely Hebrew or Aramaic, on a piece of aged, stained parchment. The text is arranged in approximately 12 horizontal lines. Several words or phrases are circled in yellow, highlighting specific parts of the text. The parchment shows signs of significant wear, including a large, irregular tear and dark staining, particularly in the lower half of the page.

Maandishi ya Zaburi ya Kitabu cha Kukunjwa cha Bahari ya Chumvi yaliyoandikwa mwanzoni mwa karne ya kwanza W.K. Maandishi hayo yameandikwa kwa kutumia herufi za Kiebrania zilizotumiwa baada ya Wayahudi kutoka utekwani Babiloni, lakini Tetragramatoni imeandikwa waziwazi tena na tena kwa herufi za kale za Kiebrania


zilizohifadhiwa tangu enzi za kabla ya Kristo, zina jina binafsi la Mungu. Kama ilivyotajwa hapo juu, Mungu aliwaongoza waandikaji kuandika jina lake mara 7,000 hivi katika Neno lake. Bila shaka, anataka tulijue na kulitumia jina lake.

- Watafsiri wanaoondoa jina hilo kwa kufuata desturi ya Kiyahudi wanakosa kuelewa jambo fulani muhimu. Ingawa waandishi fulani Wayahudi waliepuka kulitamka jina hilo, hawakuliondoa kwenye nakala zao za Biblia. Vitabu vya kukunjwa vya kale vilivyopatikana huko Qumran, karibu na Bahari ya Chumvi, vina jina hilo katika sehemu nyingi. Watafsiri fulani wa Biblia wanadokeza kwamba jina la Mungu lilipatikana katika maandishi ya awali kwa kuandika jina la cheo “BWANA” kwa herufi kubwa. Lakini huenda tukajiuliza, Kwa nini watafsiri hao waliamua kutumia jina la cheo au kuondoa jina la Mungu katika Biblia ingawa wanakubali kwamba linapatikana katika maandishi ya Biblia mara nyingi? Ni nani aliyewapa mamlaka ya kufanya mabadiliko hayo? Wao ndio wanaojua.
- Wale wanaosema kwamba jina la Mungu halipaswi kutumiwa kwa sababu haijulikani hasa jinsi lilivyotamkwa, wanatumia jina la Yesu kwa uhuru. Hata hivyo, wanafunzi wa Yesu katika karne ya kwanza walitamka jina lake tofauti na jinsi Wakristo wengi wanavyolitamka leo. Huenda Wakristo Wayahudi walilitamka jina Yesu, *Ye-shu’a*. Na kuhusu jina la cheo “Kristo” walitumia *Ma-shi’ach*, au “Masihi.” Wakristo waliozungumza Kigiriki walimwita *I-e-sous’ Khri-stos’*, na Wakristo waliozungumza Kilatini walimwita *le’sus Chri’stus*. Kwa mwongozo wa roho takatifu, tafsiri ya Kigiriki ya jina lake iliandikwa katika Biblia, na hivyo kuonyesha kwamba Wakristo wa karne ya kwanza walitumia busara kwa kutumia jina lililotumiwa na watu wengi katika lugha yao. Vivyo hivyo, Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya inaamini kwamba ni jambo la busara kutumia jina “Yehova,” ingawa huenda jina la Mungu lilitamkwa kwa njia tofauti katika Kiebrania cha kale.

Kwa nini Tafsiri ya Ulimwengu Mpya inatumia jina “Yehova”? Katika Kiswahili, herufi nne za Tetragramatoni (יהוה) zinawakilishwa na konsonanti *YHWH*. Kama ilivyokuwa na maneno yote yaliyoandikwa katika Kiebrania cha kale, Tetragramatoni haikuwa na vokali. Katika matamshi yao ya kawaida, wasomaji wa Kiebrania cha kale waliongeza vokali zifaazo.

Karibu miaka elfu moja baada ya Maandiko ya Kiebrania kukamilishwa, wasomi Wayahudi walibuni alama za matamshi, au ishara, ambazo zilionyesha vokali zilizotumiwa kusoma Kiebrania. Hata hivyo, wakati huo Wayahudi wengi walikuwa na mawazo

Jina la Mungu
kwenye Mwanzo
15:2 katika tafsiri
ya William Tyndale
ya Pentateuki, 1530



ya kishirikina kwamba ni makosa kutaja jina la Mungu kwa sauti, basi walitumia majina ya badala. Hivyo, inaonekana kwamba waliponakili Tetragramatoni, waliunganisha vokali za *majina* ya *badala* pamoja na zile konsonanti nne zinazowakilisha jina la Mungu. Kwa hiyo, hati za awali zenye alama hizo za matamshi hazuwezi kutusaidia kujua jinsi jina hilo lilivyotamkwa mwanzoni katika Kiebrania. Watu fulani husema kwamba jina hilo lilitamkwa “Yahweh,” huku wengine wakiwa na maoni tofauti. Kitabu fulani cha kukunjwa cha Bahari ya Chumvi kina kishemua cha kitabu cha Mambo ya Walawi cha Kigiriki kilichotohoa jina la Mungu kuwa *lao*. Zaidi ya kutumia *lao*, waandikaji wa kale wa Kigiriki wanadokeza pia matamshi kama *lae*, *l-a-be’*, na *l-a-ou-e’*. Hata hivyo hakuna sababu ya kuweka sheria. Kwa kweli hatujui jinsi watumishi wa kale wa Mungu walivyotamka jina hili katika Kiebrania. (Mwanzo 13:4; Kutoka 3:15) Tunachojua ni kwamba Mungu alitumia jina lake mara nyingi alipozungumza na watu wake, na kwamba walimwita kwa kutumia jina hilo, na walilitumia kwa uhuru katika mazungumzo yao.—Kutoka 6:2; 1 Wafalme 8:23; Zaburi 99:9.

Hivyo basi, kwa nini tafsiri hii inatumia jina “Yehova”? Kwa sababu jina hilo la Mungu limetumiwa kwa miaka mingi sana katika lugha ya Kiswahili.

Pia, jina hilo limeandikwa kwa njia mbalimbali katika lugha nyingine, kwa mfano, jina la Mungu lilitumiwa kwa mara ya kwanza katika Biblia ya Kiingereza mwaka wa 1530 katika tafsiri ya William Tyndale ya Pentateuki. Alitumia jina “*Iehouah*.” Baada ya muda, lugha ya Kiingereza ilibadilika, na herufi za jina la Mungu zikaboreshwa. Kwa mfano, mwaka wa 1612, Henry Ainsworth alitumia jina “*Iehovah*” alipotafsiri kitabu chote cha Zaburi. Kisha, mwaka wa 1639, tafsiri hiyo ilipofanyiwa marekebisho na kuchapishwa pamoja na Pentateuki, jina “*Jehovah*” lilitumiwa. Mwaka

wa 1901, watafsiri waliotokeza Biblia ya *American Standard Version* walitumia jina “*Jehovah*” mahali palipokuwa na jina la Mungu katika maandishi ya Kiebrania.

Akieleza sababu iliyofanya atumie jina “*Jehovah*” badala ya “*Yahweh*” katika kitabu chake *Studies in the Psalms*, cha 1911, msomi aliyeheshimiwa wa Biblia Joseph Bryant Rotherham alisema kwamba alitaka kutumia “jina ambalo lilitumiwa zaidi (na kukubaliwa kabisa) na wasomaji wengi wa Biblia.” Mwaka wa 1930 msomi A. F. Kirkpatrick alisema jambo kama hilo kuhusu matumizi ya jina “*Jehovah*.” Alisema hivi: “Wasomi wa kisasa wa lugha wanadai kwamba linapaswa kuandikwa *Yahveh* au *Yahaveh*; lakini inaonekana *JEHOVAH* ndilo linalotumika zaidi katika Kiingereza, na jambo muhimu si kujua matamshi kamili, bali kutambua kwamba ni Jina Binafsi, tofauti na jina la cheo kama vile ‘Bwana.’” Katika Biblia nyingi za Kiswahili, jina la Mungu huandikwa “Yehova.”

Jina Yehova linamaanisha nini? Katika Kiebrania, jina Yehova linatokana na kitenzi kinachomaanisha “kuwa,” na wasomi fulani wanafikiri kwamba ni kitenzi kisababishi katika lugha ya Kiebrania. Hivyo basi, kulingana na Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya jina la Mungu linamaanisha “Yeye Husababisha Kuwa.” Wasomi wana maoni mbalimbali, na hivyo hatuwezi kusisitiza maana hiyo. Hata hivyo, ufafanuzi huo unafaa kabisa kuhusiana na jukumu la Yehova akiwa Muumba wa vitu vyote na Mtimizaji wa kusudi lake. Mbali na kuumba ulimwengu na viumbe wenye akili, kadiri muda unavyosonga, ndivyo anavyoendelea kutimiza mapenzi na kusudi lake.

Kwa hiyo, maana ya jina Yehova haihusiani tu na kitenzi kilicho kwenye andiko la Kutoka 3:14 linalosema: “Nitakuwa Kile Ninachochagua Kuwa” au “Nitathibitika Kuwa Kile Nitakachothibitika Kuwa.” Ukweli ni kwamba maneno hayo ni sehemu tu ya maana kamili ya jina la Mungu. Yaani, yanafunua jambo fulani kuhusu utu wa Mungu, yakionyesha kwamba yeye huwa chochote kinachohitajika katika kila hali ili kutimiza kusudi lake. Kwa hiyo, ingawa huenda jina Yehova linatia ndani maana hiyo, jina hilo halimaanishi tu kile anachoamua kuwa. Pia, linatia ndani mambo anayosababisha yataendeke kuhusiana na uumbaji wake na kutimizwa kwa kusudi lake.

יהוה

Tetragramatoni,
YHWH: “Yeye
Husababisha
Kuwa”

יהוה

Kitenzi HWH:
“kuwa”

Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo

Wasomi wa Biblia wanakubali kwamba jina binafsi la Mungu, linalowakilishwa na Tetragramatoni (יהוה), linapatikana karibu mara 7,000 katika maandishi ya awali ya Maandiko ya Kiebrania. Hata hivyo, wengi wanahisi kwamba halikupatikana katika maandishi ya awali ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Kwa hiyo, tafsiri nyingi za kisasa za Biblia ya Kiswahili hazitumii jina Yehova katika sehemu inayoitwa Agano Jipya. Hata wanapotafsiri sehemu zilizokuliwa za Maandiko ya Kiebrania ambapo Tetragramatoni ilipatikana, watafsiri wengi hutumia jina “Bwana” badala ya jina binafsi la Mungu.

Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya haifuati mtindo huo wa kutafsiri. Inatumia jina Yehova mara 237 katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Walipoamua kufanya hivyo, watafsiri walifikiria mambo mawili muhimu: (1) Hati za Kigiriki tulizo nazo leo si hati za awali kabisa. Kati ya maelfu ya nakala zilizopo leo, nyingi ziliandikwa miaka mia mbili hivi baada ya nakala za kwanza kuandikwa. (2) Wakati huo, wale walionakili hati za kale walibadili Tetragramatoni na kutumia *Ky’ri-os*, neno la Kigiriki linaloamaanisha “Bwana,” au walinakili kutoka kwa hati ambazo tayari zilikuwa zimebadili jina la Mungu.


Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya iliamua kwamba kuna uthibitisho wa kutosha kuwa Tetragramatoni ilipatikana katika hati za awali za Kigiriki. Uamuzi huo ulitegemea uthibitisho ufuatao:

- **Nakala za Maandiko ya Kiebrania zilizotumiwa katika siku za Yesu na mitume wake zilikuwa na Tetragramatoni kote kote katika Maandiko.** Zamani watu fulani walipinga hoja hiyo. Kwa kuwa sasa nakala za Maandiko ya Kiebrania zilizoandikwa katika karne ya kwanza zimepatikana karibu na Qumran, jambo hilo limethibitishwa kikamili.
- **Katika siku za Yesu na mitume wake, Tetragramatoni ilipatikana pia katika tafsiri za Kigiriki za Maandiko ya Kiebrania.** Kwa karne nyingi, wasomi walifikiri kwamba Tetragramatoni haikupatikana katika hati za Septuajinti, yaani, tafsiri ya Kigiriki ya Maandiko ya Kiebrania. Kisha, katikati ya karne ya 20, wasomi walipata vipande fulani vya kale sana vya Septuajin-


ti ya Kigiriki ambavyo vilitumiwa katika siku za Yesu. Vipande hivyo vina jina binafsi la Mungu, likiwa limeandikwa kwa herufi za Kiebrania. Basi katika siku za Yesu, nakala za Maandiko ya Kigiriki zilikuwa na jina la Mungu. Hata hivyo, kufikia karne ya nne W.K., hati kuu za *Septuajinti* ya Kigiriki, kama vile Kodeksi ya Vatikani na Kodeksi ya Sinai, hazikuwa na jina la Mungu kuanzia kitabu cha Mwanzo hadi Malaki (ingawa hati za awali zilikuwa na jina hilo). Hivyo, haishangazi kuona kwamba nakala zilizohifadhiwa za wakati huo, hazina jina la Mungu katika sehemu inayoitwa Agano Jipya, au Maandiko ya Kigiriki katika Biblia.

- **Maandiko ya Kigiriki yanaripoti kwamba Yesu alitumia jina la Mungu mara nyingi na kuwajulisha wengine kulihusu.** (Yohana 17:6, 11, 12, 26) Yesu alisema hivi waziwazi: “Nimekuja katika jina la Baba yangu.” Pia, alikazia kwamba alifanya kazi katika “jina la Baba” yake.—Yohana 5:43; 10:25.
- **Kwa kuwa Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo yaliyoongozwa na roho ya Mungu yaliiongezwa kwenye Maandiko matakatifu ya Kiebrania, haingewezekana jina la Mungu liondolewe ghafula.** Katika karne ya kwanza W.K., mwanafunzi Yakobo aliwaambia hivi wazee huko Yerusalemu: “Simioni amesimulia kikamili jinsi Mungu kwa mara ya kwanza alivyoelekeza uangalifu wake kwa mataifa ili achukue kutoka kwao watu kwa ajili ya jina lake.” (Matendo 15:14) Yakobo hangesema maneno hayo ikiwa hakuna mtu yeyote katika karne ya kwanza ambaye alijua au kutumia jina la Mungu.
- **Jina la Mungu limeandikwa kwa ufupisho katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.** Kwenye andiko la Ufunuo 19:1, 3, 4, 6, jina la Mungu linapatikana katika neno “Haleluya.” Neno hilo linatokana na maneno ya Kiebrania yanayomaanisha “Msifuni Yah.” “Yah” ni ufupisho wa jina Yehova. Majina mengi yaliyotumiwa katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo yalitokana na jina la Mungu. Kwa kweli, utafiti unaonyesha kwamba jina Yesu linamaanisha “Yehova Ni Wokovu.”
- **Maandishi ya kale ya Wayahudi yanaonyesha kwamba Wakristo Wayahudi walitumia jina la Mungu katika maandishi yao.** Mkusanyo wa sheria unaoitwa *Tosefta*, ambao ulikamilishwa


Yesu alisema hivi waziwazi: “Nimekuja katika jina la Baba yangu.” Pia, alikazia kwamba alifanya kazi katika “jina la Baba” yake





Kumbukumbu la Torati 6:4
Mafunjo ya Nash
Karne ya pili au ya kwanza K.W.K.



Kishehu cha Kumbukumbu la Torati 18:15, 16
P. Fouad Inv. 266
Karne ya kwanza K.W.K.



Kumbukumbu la Torati 18:15, 16
Kodeksi ya Alexandria
Karne ya tano W.K.



Andiko la Matendo 3:22, likinukuu
Kumbukumbu la Torati 18:15
Tafsiri ya Ulimwengu Mpya
Karne ya 20 W.K.

Maandishi ya kale ya Kiebrania
yenye jina la Mungu mara mbili

Tafsiri ya Septuajinti ya Kigiriki
ikiwa na jina la Mungu katika
herufi za Kiebrania

Jina la Mungu likiwa
limeondolewa na badala yake
kuwekwa herufi KC na KY,
ambao ni ufupisho wa neno
la Kirigiki *Ky'ri-os* (Bwana)


Tafsiri ya Ulimwengu Mpya
imerudisha jina la Mungu

karibu mwaka wa 300 W.K., unasema hivi kuhusu maandishi ya Wakristo yaliyoteketewa siku ya Sabato: “Wanavitekeza vitabu vya Waeneza Injili na vitabu vya *minim* [watu wanaodhaniwa kuwa Wakristo Wayahudi]. Vinateketewa popote vinapopatikana, pamoja na marejeo ya Jina la Mungu lililo katika vitabu hivyo.” Maandishi hayo pia yanamnukuu Mgalilaya anayelitwa Rabi Yosé aliyeishi mwanzoni mwa karne ya pili W.K., akisema kwamba katika siku nyingine za juma “mtu hukata marejeo ya Jina la Mungu [katika maandishi ya Kikristo] na kuyahifadhi, kisha anateketeza maandishi yanayobaki.”

- Baadhi ya wasomi wa Biblia wanasema inawezekana kwamba jina la Mungu lilipatikana katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo kwenye sehemu zilizozitakiwa Maandiko ya Kiebrania. Kamusi ya *The Anchor Bible Dictionary* chini ya kichwa “Tetragramatoni Katika Agano Jipya,” inasema: “Kuna uthibitisho kwamba, maandishi ya Agano Jipya yalipoandikwa kwa mara ya kwanza, Tetragramatoni, Jina la Mungu, Yahweh, ilipatikana katika baadhi au sehemu zote za Agano la Kale zilizozitakiwa katika Agano Jipya.” Msomi George Howard anasema hivi: “Kwa kuwa bado Tetragramu iliandikwa katika nakala za Biblia ya Kigiriki [*Septuajinti*] iliyofanyiza Maandiko ya kanisa

la awali, ni jambo la busara kuamini kwamba waandishi wa Agano Jipya walitumia Tetragramu katika Biblia waliponukuu Maandiko.”

- **Watafsiri maarufu wa Biblia wametumia jina la Mungu katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.** Baadhi ya watafsiri hao walifanya hivyo muda mrefu kabla ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* kuchapishwa. Tafsiri hizo zinatia ndani *A Literal Translation of the New Testament . . . From the Text of the Vatican Manuscript*, ya Herman Heinfetter (1863); *The Emphatic Diaglott*, ya Benjamin Wilson (1864); *The Epistles of Paul in Modern*




Jina la Mungu kwenye Matendo 2:34 katika tafsiri ya *The Emphatic Diaglott*, ya Benjamin Wilson (1864)

English, ya George Barker Stevens (1898); *St. Paul's Epistle to the Romans*, ya W. G. Rutherford (1900); *The New Testament Letters*, ya J.W.C. Wand, Askofu wa London (1946). Isitoshe, katika tafsiri ya Kihispania mwanzoni mwa karne ya 20, mtafsiri Pablo Besson alitumia jina “*Jehová*” kwenye Luka 2:15 na Yuda 14, na zaidi ya mara 100 katika maelezo ya chini ya tafsiri yake. Muda mrefu kabla ya tafsiri hizo, tafsiri za Kiebrania za Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo kuanzia karne ya 16 na kuendelea zilitumia Tetragramatoni katika sehemu nyingi. Katika Kijerumani peke yake, karibu tafsiri 11 zinatumia jina

“Yehova” (au “Yahweh” kama linavyotoholewa kutoka katika Kiebrania) katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo, na watafsiri wanne waliongeza jina hilo katika mabano baada ya jina “Bwana.” Zaidi ya tafsiri 70 za Kijerumani zinatumia jina la Mungu katika maelezo ya chini au katika marejeo.

- **Tafsiri za Biblia katika lugha zaidi ya 100 zina jina la Mungu katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo.** Lugha nyingi za Afrika, za wenyeji wa asili wa Amerika, Asia, Ulaya, na visiwa vya Pasifiki zinatumia jina la Mungu mara nyingi. (Ona orodha iliyo kwenye ukurasa wa 2062 na 2063.) Watafsiri wa matoleo hayo waliamua kutumia jina la Mungu kwa sababu zinazofanana na zile zilizotajwa hapo juu. Baadhi ya tafsiri hizo za Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo zimechapishwa hivi karibuni, kama vile Biblia ya Kiroshima (1999), inayotumia jina “*Jihova*” mara 51 katika mistari 48, na tafsiri ya Batak (Toba) ya Indonesia (1989), inayotumia jina “*Jahowa*” mara 110.

Bila shaka, kuna msingi thabiti wa kurudisha jina la Mungu, Yehova, katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Hivyo ndivyo walivyofanya watafsiri wa Biblia ya *Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*. Wanalishimu sana jina la Mungu na kwa kufaa wanaogopa kuondoa chochote kilichokuwa kimeandikwa katika maandishi ya awali. —Ufunuo 22:18, 19.



Jina la Mungu kwenye Marko 12:29, 30 katika tafsiri ya Kihawaii

Lugha na Lahaja Zilizo na Jina la Mungu Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo

Lugha au Lahaja: Jina la Mungu

Kianeityum: **Ihova**
Kiarawak: **Jehovah**
Kiawabakal: **Yehóa**
Kibangi: **Yawe**
Kibatak (Toba): **Jahowa**
Kibenga: **Jéhova**
Kibolia: **Yawe**
Kibube: **Yehovah**
Kibullom So: **Jehovah**
Kichácobo: **Jahué**
Kicherokee: **Yihowa**
Kichin (Hakha): **Zahova**
Kichippewa: **Jehovah**
Kichoctaw: **Chihowa**
Kichuukese: **Jiowa**
Kidakota: **Jehowa**
Kidobu: **leoba**
Kidouala: **Yehowa**
Kiebrania: יהוה
Kiefate (Kaskazini): **Yehova**
Kiefik: **Jehovah**
Kiéwé: **Yehowa**
Kifang: **Jehôva**
Kifaransa: **IHVH, yhwh**
Kifiji: **Jiowa**
Kiga: **lehowa**
Kigibario (lahaja ya Kikerewo): **lehova**
Kigrebo: **Jehova**
Kihawaii: **lehova**
Kihindustani: **Yihováh**
Kihiri Motu: **lehova**
Kihispania: **Jehová; Yahvé; YHWH; Yahweh**
Kiho-Chunk (Winnebago): **Jehowa**

Kiholanzi: **Jehovah**
Kiila: **Yaave**
Kiiliku (lahaja ya Kilusengo): **Yawe**
Kiindonesia: **YAHWEH**
Kiingereza: **Jehovah**
Kijaluo: **Yawe**
Kijerumani: **Jehovah; Jehova**
Kikala Lagaw Ya: **lehovan**
Kikalanga: **Yehova; Yahwe**
Kikalenjin: **Jehovah**
Kikerewo: **lehova**
Kikorea: **여호와**
Kikosrae: **Jeova**
Kikroatia: **Jehova**
Kikuanua: **leova**
Kilaotia: **Yehowa**
Kilele: **Jehova**
Kilewo: **Yehova**
Kilogo: **Yehova**
Kilomongo: **Yawe; Yova**
Kilonwolwol: **Jehovah**
Kiluba: **Yehova**
Kilugbara: **Yehova**
Kiluimbi: **Yehova**
Kiluna: **Yeoba**
Kilunda: **Yehova**
Kiluvale: **Yehova**
Kimalagasi: **Jehovah; lehôvah**
Kimalo: **Iova**
Kimarquesa: **lehova**
Kimarshall: **Jeova**
Kimaskelyne: **Iova**
Kimentawai: **Jehoba**
Kimeriam: **lehoua**

Kimisima-Paneati: **Iehova**
 Kimizo: **Jehovan; Jihova'n**
 Kimohawk: **Yehovah**
 Kimortlock: **Jioua**
 Kimotu: **Iehova**
 Kimpongwe (lahaja ya Kimyene): **Jehova**
 Kimuskoge: **Cehofv**
 Kimyene: **Yeōva**
 Kinaga, Kiangami: **Jihova**
 Kinaga, Kikonyak: **Jihova**
 Kinaga, Kilotha: **Jihova**
 Kinaga, Kimao: **Jihova**
 Kinaga, Rengma Kaskazini: **Jihova**
 Kinaga, Sangtam: **Jihova**
 Kinandi: **Jehova**
 Kinarrinyeri: **Jehovah**
 Kinauru: **Jehova**
 Kinavajo: **Jiho'vah**
 Kindau: **Jehova**
 Kinembe: **Jehovah**
 Kinengone (au, Kimaré): **Iehova**
 Kingala: **Yawe**
 Kingando: **Yawe**
 Kintomba: **Yawe**
 Kinukuoro: **Jehova**
 Kipolandi: **Jehowa**
 Kipsigis: **Jehoba**
 Kirarotonga: **Jehova; Iehova**
 Kireno: **Iáhve**
 Kirerep: **Iova**
 Kiribati: **Iehova**
 Kirotuman: **Jihova**
 Kisakao: **Ihova; Iehova**
 Kisamoā: **Ieova**


Kiseneka: **Ya'wēn**
 Kisengele: **Yawe**
 Kisesofo: **Yehofa**
 Kisie: **Iehōva**
 Kisonge: **Yehowa**
 Kisranantongo: **Jehova**
 Kisukuma: **Yahuwa; Jakwe**
 Kitahiti: **Iehova**
 Kiteke-Eboo: **Yawe**
 Kitemne: **Yehōfa; Yehofa**
 Kithai: **Yahowa**
 Kitoaripi: **Jehova; Iehova**
 Kitonga: **Jehova**
 Kitongan: **Jihova; Sihova**
 Kitshiluba: **Yehowa**
 Kitswana: **Jehofa; Yehova; Yehofa**
 Kiumbundu: **Yehova**
 Kiuripiv: **Iova**
 Kiwampanoag: **Jehovah**
 Kiwelsh: **Iehofah**
 Kixhosa: **Yehova**
 Kizande: **Yekova**
 Kizulu: **Jehova; YAHWE**

(Lugha na lahaja nyingine zisizo kwenye orodha hii hutumia jina la Mungu kwenye maelezo ya chini au kwenye maandishi ya ufafanuzi.


Zaidi ya lugha 120

Chati: Manabii na Wafalme wa Yuda na Israeli

Wafalme wa Ufalme wa **Kusini** wa Yuda Uliokuwa na Makabila Mawili



Wafalme wa Ufalme wa **Kaskazini** wa Israeli Uliokuwa na Makabila Kumi



Wafalme wa Ufalme wa Kusini
(Imeendelezwa)

Uzia (Azaria): Miaka 52

Yothamu: Miaka 16

Ahazi: Miaka 16

Hezekia: Miaka 29

Manase: Miaka 55

Amoni: Miaka 2

Yosia: Miaka 31


Yehoahazi: Miezi 3

Yehoyakimu: Miaka 11


Yehoyakini: Miezi 3, siku 10

Sedekia: Miaka 11

Jiji la Yerusalemu na hekalu lake laharibiwa na majeshi ya Wababiloni yakiongozwa na Nebukadnezar. Sedekia, mfalme wa mwisho wa kidunia katika ukoo wa Daudi, aondolewa mamlakani



Wafalme wa Ufalme wa Kaskazini
(Imeendelezwa)



Matukio Muhimu Katika Maisha ya Yesu Duniani

Vitabu Vinne vya Injili Kulingana na Mfuatano wa Matukio

Chati zifuatazo zina ramani zinazoonyesha safari za kuhubiri za Yesu. Mishale kwenye ramani haionyeshi njia hususa aliyofuata badala yake inaonyesha alikoelekea.


Matukio Yaliyotangulia Huduma ya Yesu

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
3 K.W.K.	Yerusalemu, hekalu	Malaika Gabrieli amtangazia Zekaria kuhusu kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji			1:5-25	
Karibu 2 K.W.K.	Nazareti; Yudea	Malaika Gabrieli amtangazia Maria kuhusu kuzaliwa kwa Yesu; Maria amtembelea Elisabeti mtu wake wa ukoo			1:26-56	
2 K.W.K.	Eneo lenye milima la Yudea	Yohana Mbatizaji azaliwa na kupewa jina; Zekaria atabiri; Yohana ataishi jangwani			1:57-80	
2 K.W.K., karibu Okt. 1	Bethlehemu	Yesu azaliwa; "Neno akawa mwili"	1:1-25		2:1-7	1:14
	Karibu na Bethlehemu; Bethlehemu	Malaika awatangazia wachungaji habari njema; malaika wamsifu Mungu; wachungaji wantembelea mtoto Yesu			2:8-20	
	Bethlehemu; Yerusalemu	Yesu atahiriwa (siku ya 8); wazazi wake wampeleka hekaluni (baada ya siku 40)			2:21-38	
1 K.W.K. au 1 W.K.	Yerusalemu; Bethlehemu; Misri; Nazareti	Wanajimu wantembelea; familia inakimbilia Misri; Herode awaua wavulana wadogo; familia yarudi kutoka Misri na waishi Nazareti	2:1-23		2:39, 40	
12 W.K., Pasaka	Yerusalemu	Yesu mwenye umri wa miaka 12 akiwa hekaluni awaliza walimu maswali			2:41-50	
	Nazareti	Arudi Nazareti; aendelea kuwatii wazazi wake; ajifunza useremala; Maria apata watoto wengine wa kiume wanne, na pia watoto wa kike (Mt 13:55, 56; Mk 6:3)			2:51, 52	
29 W.K., majira ya kuchipua	Nyikani, Mto Yordani	Yohana Mbatizaji aanza huduma yake	3:1-12	1:1-8	3:1-18	1:6-8

Ramani ya 1

Alama za Ramani

- ⊕ Mwanzo
- Eneo Hususa
- Huenda ni Hapa
- ? Haijulikani kihususa



Mwanzo wa Huduma ya Yesu

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
29, Majira ya kupukutika	Mto Yordani, ng'ambo ya Yordani karibu na au huko Bethania	Yesu abatizwa na kutiwa mafuta; Yehova atangaza kwamba Yesu ni mwanawe na kumkubali	3:13-17	1:9-11	3:21-38	
	Nyika ya Yudea	Yesu ajaribiwa na Ibilisi	4:1-11	1:12, 13	4:1-13	
	Bethania ng'ambo ya Yordani	Yohana Mbatizaji amtambulisha Yesu kuwa Mwana-Kondoo wa Mungu; wanafunzi wa kwanza wajiunga na Yesu				1:15, 19-51
	Kana ya Galilaya; Kapernaumu	Muujiza wa kwanza kwenye harusi, Yesu ageuza maji kuwa divai; atembelea Kapernaumu				2:1-12
30, Pasaka	Yerusalemu	Asafisha hekalu Azungumza na Nikodemo				2:13-25 3:1-21
	Yudea; Ainoni	Yesu atembelea eneo la Yudea, wanafunzi wake wabatiza watu; ushahidi wa mwisho wa Yohana kumhusu Yesu				3:22-36
	Tiberia; Yudea	Yohana afungwa gerezeni; Yesu aondoka kuelekea Galilaya	4:12; 14:3-5	6:17-20	3:19, 20	4:1-3
	Sikari, eneo la Samaria	Akiwa njiani kwenda Galilaya, afundisha Wasamaria				4:4-43




Nyika ya Yudea

Ramani ya 2





WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
30	Galilaya	Kwanza Yesu atangaza hivi "Ufalme wa mbinguni umekaribia"	4:17	1:14, 15	4:14, 15	4:44, 45
	Kana; Nazareti; Kapernaumu	Amponya mwana wa mtawala; asoma kutoka kwenye kitabu cha Isaya; aenda Kapernaumu	4:13-16		4:16-31	4:46-54
	Bahari ya Galilaya, karibu na Kapernaumu	Awaita wanafunzi wanne: Simoni na Andrea, Yakobo na Yohana	4:18-22	1:16-20	5:1-11	
	Kapernaumu	Amponya mama-mkwe wa Simoni na wengine	8:14-17	1:21-34	4:31-41	
	Galilaya	Ziara ya kwanza ya Galilaya, na wanafunzi wanne	4:23-25	1:35-39	4:42, 43	
		Amponya mwenye ukoma; umati wamfuata	8:1-4	1:40-45	5:12-16	
	Kapernaumu	Amponya mtu aliyepooza	9:1-8	2:1-12	5:17-26	
		Amwita Mathayo; ala pamoja na wakusanya kodi; aulizwa kuhusu kufunga	9:9-17	2:13-22	5:27-39	
	Yudea	Afundisha kwenye masinagogi			4:44	
31, Pasaka	Yerusalemu	Amponya mgonjwa huko Bethzatha; Wayahudi wataka kumuua				5:1-47
	Arudi kutoka Yerusalemu (?)	Wanafunzi wachuma masuke ya ngano siku ya Sabato; Yesu "Bwana wa Sabato"	12:1-8	2:23-28	6:1-5	
	Galilaya; Bahari ya Galilaya	Aponya mkono wa mtu siku ya Sabato; umati wamfuata; aponya watu wengi zaidi	12:9-21	3:1-12	6:6-11	
	Mlimani karibu na Kapernaumu	Achagua mitume 12		3:13-19	6:12-16	
	Karibu na Kapernaumu	Mahubiri ya Mlimani	5:1-7:29		6:17-49	
	Kapernaumu	Amponya mtumishi wa ofisa wa jeshi	8:5-13		7:1-10	
	Naini	Amfufua mwana wa mjane			7:11-17	
	Tiberia; Galilaya (Naini au karibu na hapo)	Yohana awatuma wanafunzi wake kwa Yesu; ukweli wafunuliwa kwa watoto; nira laini	11:2-30		7:18-35	
	Galilaya (Naini au karibu na hapo)	Mwanamke mtenda dhambi amimina mafuta kwenye miguu ya Yesu; mfano wa watu wawili wanaodaiwa			7:36-50	
	Galilaya	Safari ya pili ya kuhubiri, akiwa na mitume 12			8:1-3	
		Afukuza roho waovu; dhambi isiyosameheka	12:22-37		3:19-30	
		Hatoishiara yoyote isipokuwa ishara ya Yona	12:38-45			
		Mama yake na ndugu zake waja; asema wanafunzi wake ndio ndugu na dada zake	12:46-50		3:31-35	8:19-21



WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
31 au 32	Eneo la Kapernaumu	Yesu asimulia mifano kuhusu Ufalme	13:1-53	4:1-34	8:4-18	
	Bahari ya Galilaya	Atuliza bahari akiwa ndani ya mashua	8:18, 23-27	4:35-41	8:22-25	
	Eneo la Gadara	Awatuma roho waovu ndani ya nguruwe	8:28-34	5:1-20	8:26-39	
	Huenda ni Kapernaumu	Amponya mwanamke mwenye mtiririko wa damu; amfufua binti ya Yairo	9:18-26	5:21-43	8:40-56	
	Kapernaumu (?)	Awaponya vipofu na mabubu	9:27-34			
	Nazareti	Akataliwa tena katika mji wa nyumbani kwao	13:54-58	6:1-5		
	Galilaya	Safari ya tatu kwenda Galilaya; apanua kazi kwa kuwatuma mitume	9:35-11:1	6:6-13	9:1-6	
	Tiberia	Herode amkata kichwa Yohana Mbatizaji; Herode ashangazwa na Yesu	14:1-12	6:14-29	9:7-9	
32, karibu na Pasaka (Yoh 6:4)	Kapernaumu (?); Kask. Mash. ya Bahari ya Galilaya	Mitume warudi kutoka safari ya kuhubiri; Yesu alisha wanaume 5,000	14:13-21	6:30-44	9:10-17	6:1-13
	Kask. Mash. ya Bahari ya Galilaya; Genesareti	Wajaribu kumfanya Yesu mfalme; atembea juu ya bahari; aponya wengi	14:22-36	6:45-56		6:14-21
	Kapernaumu	Asema yeye ndiye "mkate wa uzima"; wengi wakwazika na kumwacha				6:22-71
32, baada ya Pasaka	Labda Kapernaumu	Afunua mapokeo ya wanadamu	15:1-20	7:1-23		7:1
	Foinike; Dekapoli	Amponya binti ya mwanamke Msirofoinike; alisha wanaume 4,000	15:21-38	7:24-8:9		
	Magadani	Akataa kutoa ishara ila ya Yona	15:39-16:4	8:10-12		

Ramani ya 3B



Matukio Karibu na Bahari ya Galilaya

(Pia inaitwa Ziwa la Genesareti au Bahari ya Tiberia)


- ❶ Atuliza dhoruba akiwa ndani ya mashua
- ❷ Awatuma roho waovu ndani ya nguruwe
- ❸ Alisha wanaume 5,000
- ❹ Atembea juu ya bahari
- ❺ Alisha wanaume 4,000
- ❻ Eneo linaloaminiwa kwamba Yesu alitoa Mahubiri ya Mlimani

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
32, baada ya Pasaka	Bahari ya Galilaya; Bethsaida	Akiwa mashuani kuelekea Bethsaida, Yesu aonya kuhusu chachu ya Mafarisayo; amponya mwanamume kipofu	16:5-12	8:13-26		
	Eneo la Kaisaria Filipi	Funguo za Ufalme; atabiri kifo na ufufuo wake	16:13-28	8:27-9:1	9:18-27	
	Inaelekea ni Mt. Hermoni	Kugeuka-sura; Yehova azungumza	17:1-13	9:2-13	9:28-36	
	Eneo la Kaisaria Filipi	Amponya mvulana aliyekuwa na roho mwovu	17:14-20	9:14-29	9:37-43	
	Galilaya	Atabiri tena kuhusu kifo chake	17:22, 23	9:30-32	9:43-45	
	Kapernaumu	Alipa kodi kwa sarafu aliyoitoa kwenye kinywa cha samaki	17:24-27			
		Mkuu katika Ufalme; mifano: kondoo aliyepotea na mtumwa asiyesamehe	18:1-35	9:33-50	9:46-50	
Galilaya-Samaria	Wakielekea Yerusalemu, awaambia wanafunzi wake wadhabihu mambo yote kwa ajili ya Ufalme	8:19-22		9:51-62	7:2-10	

Huduma ya Yesu ya Baadaye Huko Yudea

32, Sherehe ya Vibanda	Yerusalemu	Afundisha kwenye Sherehe; maofisa watumwa ili kumkamata				7:11-52
		Asema: "Mimi ndiye nuru ya ulimwengu"; amponya mtu aliyezaliwa kipofu				8:12-9:41
	Inaelekea ni Yudea	Awatuma wale 70; warudi wakishangilia			10:1-24	
	Yudea; Bethania	Mfano wa Msamaria mwema; Awatembelea Maria na Martha nyumbani			10:25-42	
	Huenda ni Yudea	Afundisha tena ile sala ya kielelezo; mfano wa rafiki aliyeeendelea kuomba			11:1-13	
		Afukuza roho waovu kwa kutumia nguvu za Mungu; atoa tena ishara ya Yona			11:14-36	
Ala pamoja na Farisayo; ashutumu unafiki wa Mafarisayo				11:37-54		
Mifano: tajiri asiye na akili na msimamizi nyumba mwaminifu				12:1-59		
	Amponya mwanamke kilema siku ya Sabato; mifano ya mbegu ya haradali na chachu			13:1-21		
32, Sherehe ya Wakfu	Yerusalemu	Mchungaji mwema na zizi la kondoo; Wayahudi wajaribu kumpiga mawe; avuka Yordani aenda Bethania				10:1-39


Ramani ya 4 Sidoni



Huduma ya Yesu ya Baadaye Mashariki mwa Yordani

Ramani ya 5

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
32, baada ya Sherehe ya Wakfu	Bethania ng'ambo ya Yordani	Aenda mahali Yohana alipokuwa akibatizia watu; wengi wamwamini Yesu				10:40-42
	Perea	Afundisha katika miji na vijiji, akisafiri kwenda Yerusalemu			13:22	
		Atoa himizo la kuingia kupitia lango jembamba; aombolezea Yerusalemu			13:23-35	
Huenda ni Perea	Huenda ni Perea	Afundisha kuhusu unyenyekevu; mifano ya mahali penye kuonekana zaidi na wageni waliotoa udhuru			14:1-24	
		Hesabu gharama ya kuwa mwanafunzi			14:25-35	
		Mifano ya kondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea, mwana mpotevu			15:1-32	
		Mifano ya msimamizi asiye mwadilifu, tajiri na Lazaro			16:1-31	
	Afundisha kuhusu kukwaza, kusamehe, na imani			17:1-10		
Bethania	Lazaro afa na kufufuliwa				11:1-46	
Yerusalemu; Efraimu	Njama ya kumuua Yesu; aondoka				11:47-54	
Samaria; Galilaya	Awaponya watu kumi wenye ukoma; aeleza jinsi Ufalme wa Mungu utakavyokuja			17:11-37		
Samaria au Galilaya	Mifano ya mjane aliyendelea kuomba, Farisayo na mkusanya-kodi			18:1-14		
Perea	Perea	Afundisha kuhusu ndoa na talaka	19:1-12	10:1-12		
		Awabariki watoto	19:13-15	10:13-16	18:15-17	
		Swali la tajiri; mfano wa wafanyakazi katika shamba la mizabibu na kiwango kilekile cha mshahara	19:16-20:16	10:17-31	18:18-30	
Inaelekea ni Perea	Inaelekea ni Perea	Atabiri kuhusu kifo chake mara ya tatu	20:17-19	10:32-34	18:31-34	
		Ombi la Yakobo na Yohana kupata cheo katika Ufalme	20:20-28	10:35-45		
Yeriko	Yeriko	Apitia huko, awaponya wanaume wawili vipofu; amtembelea Zakayo; mfano wa mina kumi	20:29-34	10:46-52	18:35-19:28	



Huduma ya Mwisho ya Yesu Kule Yerusalemu

Ramani ya 6

WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA	
33, Nisani 8	Bethania	Yesu awasili siku sita kabla ya Pasaka				11:55 – 12:1	
Nisani 9	Bethania	Maria ammininia Yesu mafuta kichwani na miguuni	26:6-13	14:3-9		12:2-11	
	Bethania-Bethfage-Yerusalemu	Aingia Yerusalemu kwa ushindi, akiwa juu ya punda	21:1-11, 14-17	11:1-11	19:29-44	12:12-19	
Nisani 10	Bethania-Yerusalemu	Aulaani mtini; alisafisha hekalu tena	21:18, 19; 21:12, 13	11:12-17	19:45, 46		
	Yerusalemu	Makuhani wakuu na waandishi wapanga njama ya kumuua Yesu		11:18, 19	19:47, 48		
		Yehova azungumza; Yesu atabiri kifo chake; kutoamini kwa Wayahudi kwatimiza unabii wa Isaya					12:20-50
Nisani 11	Bethania-Yerusalemu	Somo la mtini ulionyauka	21:19-22	11:20-25			
	Yerusalemu, hekalu	Mamlaka yake yatiliwa shaka; mfano wa wana wawili	21:23-32	11:27-33	20:1-8		
		Mifano ya wakulima wauaji wa shamba la mizabibu, karamu ya ndoa	21:33-22:14	12:1-12	20:9-19		
		Ajibu maswali kumhusu Mungu na Kaisari, ufufuo, sheria iliyo kuu zaidi	22:15-40	12:13-34	20:20-40		
		Auuliza umati ikiwa Kristo ni mwana wa Daudi	22:41-46	12:35-37	20:41-44		
		Ole kwa waandishi na Mafarisayo	23:1-39	12:38-40	20:45-47		
		Aona mchango wa mjane		12:41-44	21:1-4		
		Mlima wa Mizeituni	Ataja ishara ya kuwapo kwake wakati ujao	24:1-51	13:1-37	21:5-38	
		Mifano ya mabikira kumi, talanta, kondoo na mbuzi	25:1-46				
	Nisani 12	Yerusalemu	Viongozi Wayahudi wapanga njama ya kumuua	26:1-5	14:1, 2	22:1, 2	
Yuda apanga jinsi atakavyomsaliti			26:14-16	14:10, 11	22:3-6		
Nisani 13 (Alhamisi alasiri)	Akiwa Yerusalemu na maeneo ya karibu	Matayarisho ya Pasaka ya mwisho	26:17-19	14:12-16	22:7-13		
Nisani 14	Yerusalemu	Ala Pasaka pamoja na mitume wake	26:20, 21	14:17, 18	22:14-18		
		Awaosha mitume wake miguu				13:1-20	



WAKATI	MAHALI	TUKIO	MATHAYO	MARKO	LUKA	YOHANA
Nisani 14	Yerusalemu	Yesu amtaja Yuda kuwa msaliti kisha amfukuza	26:21-25	14:18-21	22:21-23	13:21-30
		Aanzisha Mlo wa Jioni wa Bwana (1Ko 11:23-25)	26:26-29	14:22-25	22:19, 20, 24-30	
		Atabiri kwamba Petro atamkana na mitume watatawanyika	26:31-35	14:27-31	22:31-38	13:31-38
		Aahidi kumtuma msaidizi; mfano wa mzabibu wa kweli; atoa amri ya kupendana; sala ya mwisho pamoja na mitume wake				14:1-17:26
	Gethsemane	Maumivu makali kwenye bustani; Yesu asalitiwa na kukamatwa	26:30, 36-56	14:26, 32-52	22:39-53	18:1-12
	Yerusalemu	Ahojiwa na Anasi; ahojiwa na Kayafa, Sanhedrini; Petro amkana	26:57-27:1	14:53-15:1	22:54-71	18:13-27
Yuda msaliti ajinyonga (Mdo 1:18, 19)		27:3-10				
Mbele ya Pilato, kisha Herode, na kurudi kwa Pilato		27:2, 11-14	15:1-5	23:1-12	18:28-38	
Pilato ataka kumwachilia lakini Wayahudi wasema wanamtaka Baraba; ahukumiwa kuuawa kwenye mti wa mateso		27:15-30	15:6-19	23:13-25	18:39-19:16	
(Karibu saa 9:00 alasiri, Ijumaa)	Golgotha	Afa kwenye mti wa mateso	27:31-56	15:20-41	23:26-49	19:16-30
	Yerusalemu	Mwili wake watolewa mtini na kuwekwa kaburini	27:57-61	15:42-47	23:50-56	19:31-42
Nisani 15	Yerusalemu	Makuhani na Mafarisayo waweka walenzi kulilinda kaburi na kulitia muhuri	27:62-66			
Nisani 16	Yerusalemu na maeneo ya karibu; Emau	Yesu afufuliwa; awatokea wanafunzi mara tano	28:1-15	16:1-8	24:1-49	20:1-25
Baada ya Nisani 16	Yerusalemu; Galilaya	Awatokea wanafunzi wake tena na tena (1Ko 15:5-7; Mdo 1:3-8); awafundisha; awatuma kufanya wanafunzi	28:16-20			20:26-21:25
Iyari 25	Mlima wa Mizeituni, karibu na Bethania	Yesu apaa mbinguni, siku 40 baada ya kufufuliwa (Mdo 1:9-12)			24:50-53	



Nyongeza B

	Ujumbe wa Biblia	B1
Ramani	Kitabu cha Mwanzo na Safari za Wazee wa Ukoo	B2
Ufunguo wa Ramani	Safari ya Kutoka Misri	B3
● Eneo Hili Limethibitishwa kwa Kadiri Fulani	Kumiliki Nchi ya Ahadi	B4
○ Eneo Hili Linatiliwa Shaka ? eneo hususa halijulikani	Maeneo ya Nchi ya Ahadi	B6
— Barabara	Ufalme wa Daudi na Sulemani	B7
Ramani zote zimechorwa kwa kutegemea upande wa kaskazini wa dira	Serikali Kuu za Ulimwengu Zilizotabiriwa na Danieli	B9
Majina yaliyotumiwa katika kipindi kilekile kurejelea eneo fulani yametenganishwa kwa kutumia kituo	Nchi ya Israeli Katika Siku za Yesu	B10
Majina yaliyotumiwa katika vipindi tofauti kurejelea eneo fulani yameandikwa katika mabano	Kuenea kwa Ukristo	B13
Michoro	Hema la Ibada na Kuhani Mkuu	B5
	Hekalu Lililojengwa na Sulemani	B8
	Hekalu la Mlimani Katika Karne ya Kwanza	B11
Wakati	Juma la Mwisho la Maisha ya Yesu Duniani	B12
	Kalenda ya Kiebrania	B15
Vipimo	Biashara	B14

Ujumbe wa Biblia

Yehova Mungu ana haki ya kutawala.

Njia yake ya kutawala ndiyo njia bora kabisa.

Kusudi lake kwa ajili ya dunia na wanadamu litatimia.



**Baada ya
4026 K.W.K.**

“Yule nyoka” atilia shaka haki ya Yehova ya kutawala na njia yake ya kutawala. Yehova aahidi kutokeza “uzao,” au “mbegu,” ambaye hatimaye atamponda yule nyoka, Shetani. (Mwanzo 3: 1-5, 15, maelezo ya chini) Hata hivyo, Yehova aruhusu muda upite ili wanadamu wajitawale chini ya uongozi wa yule nyoka.



**1943
K.W.K.**

Yehova amwambia Abrahamu kwamba “uzao” ulioahidiwa utatoka miongoni mwa wazao wake.—Mwanzo 22:18.



**Baada ya
1070 K.W.K.**

Yehova amhakikishia Mfalme Daudi na baadaye Sulamani mwanawe kwamba “uzao” ulioahidiwa ungetokea kwenye ukoo wao.—2 Samweli 7: 12, 16; 1 Wafalme 9:3-5; Isaya 9:6, 7.



**29
W.K.**

Yehova amtambulisha Yesu kuwa “uzao” ulioahidiwa na Mrithi wa kiti cha ufalme cha Daudi.—Wagalatia 3:16; Luka 1:31-33; 3:21, 22.



**33
W.K.**

Yule nyoka, Shetani, aujeruhi kwa muda mfupi ule “uzao” ulioahidiwa kwa kusababisha Yesu auawe. Yehova amfufua Yesu akaishi mbinguni, naye akubali thamani ya uhai mkamilifu wa Yesu, na hivyo kuweka msingi wa kusamehe dhambi na kuwapa wazao wa Adamu uzima wa milele.—Mwanzo 3:15; Matendo 2:32-36; 1 Wakorintho 15: 21, 22.



**Karibu
1914 W.K.**

Yesu amvurumisha duniani yule nyoka, Shetani, na kumzuia humo kwa muda mfupi.—Ufunuo 12:7-9, 12.



**Wakati
Ujao**

Yesu amfungua Shetani kwa miaka 1,000 kisha amwangamiza, na hivyo kumponda kichwa kwa njia ya mfano. Kusudi la Yehova la awali kwa ajili ya dunia na wanadamu litatimia, jina lake laondolewa suto na njia yake ya kutawala yatetewa.—Ufunuo 20:1-3, 10; 21:3, 4.

Kitabu cha Mwanzo na Safari za Wazee wa Ukoo

Adamu aumbwa 4026 K.W.K.
Agano la Kiabrahamu lalalishwa 1943 K.W.K.
Yosefu afa 1657 K.W.K.

4000 K.W.K. 2000 K.W.K. K.W.K. / W.K. 2000 W.K.



BAHARI KUU

PADAN-ARAMU

ASHURU

M E S O P O T A M I A

ELAMU

S H I N A R I (BABILONIA)

UKALDAYO

K A N A A N I

MOABU



EDOMU, SEIRI

MISRI



0 maili 100
0 kilomita 100

Hema la Ibada na Kuhani Mkuu




Sehemu za Hema la Ibada

- 1 Sanduku la Agano (Kut 25:10-22; 26:33)
- 2 Pazia (Kut 26:31-33)
- 3 Nguzo za Pazia (Kut 26:31, 32)
- 4 Patakatifu (Kut 26:33)
- 5 Patakatifu Zaidi (Kut 26:33)
- 6 Pazia (Kut 26:36)
- 7 Nguzo za Pazia (Kut 26:37)
- 8 Vikalio vya Shaba (Kut 26:37)
- 9 Madhabahu ya Uvumba (Kut 30:1-6)
- 10 Meza ya Mikate ya Wonyesho (Kut 25:23-30; 26:35)
- 11 Kinara cha Taa (Kut 25:31-40; 26:35)
- 12 Kitambaa cha Hema cha Kitani (Kut 26:1-6)
- 13 Kitambaa cha Hema cha Manyoya ya Mbuzi (Kut 26:7-13)
- 14 Kifuniko cha Ngozi za Kondoo Dume (Kut 26:14)
- 15 Kifuniko cha Ngozi za Sili (Kut 26:14)
- 16 Kiunzi cha Mbao (Kut 26:15-18, 29)
- 17 Kikalio cha Fedha Chini ya Kiunzi (Kut 26:19-21)
- 18 Ufito (Kut 26:26-29)
- 19 Kikalio cha Fedha (Kut 26:32)

Kuhani Mkuu

Kutoka sura ya 28 inafanua kwa kina mavazi ya kuhani mkuu wa Israeli



- 1 Kilemba (Kut 28:39)
- 2 Ishara Takatifu ya Wakfu (Kut 28:36; 29:6)
- 3 Jiwe la Shohamu (Kut 28:9)
- 4 Mnyororo (Kut 28:14)
- 5 Kifuko cha Kifuni cha Maa-muzi Chenye Mawe 12 Yenye Thamani (Kut 28:15-21)
- 6 Efodi na Mshipi Wake Uliofu-mwa (Kut 28:6, 8)
- 7 Joho la Bluu Lisilo na Mikono (Kut 28:31)
- 8 Upindo Wenye Kengele na Makomamanga (Kut 28:33-35)
- 9 Kanzu ya Kitani Bora Yenye Miraba (Kut 28:39)




20



21

- 20 Beseni la Shaba (Kut 30:18-21)
- 21 Madhabahu ya Dhabihu za Kuteketezwa (Kut 27:1-8)
- 22 Ua (Kut 27:17, 18)
- 23 Mlango (Kut 27:16)
- 24 Mapazia ya Kitani Yali-ying'inia (Kut 27:9-15)



Maeneo ya Nchi ya Ahadi

Makabila yapewa ardhi baada ya kushinda vita 1467 K.W.K. Sauli atiwa mafuta kuwa mfalme 1117 K.W.K.

4000 K.W.K. 2000 K.W.K. K.W.K. / W.K. 2000 W.K.

Waamuzi

- 1 Othnieli
- 2 Ehudi
- 3 Shamgari
- 4 Baraka
- 5 Gideon
- 6 Tola
- 7 Yairi
- 8 Yeftha
- 9 Ibzani
- 10 Eloni
- 11 Abdoni
- 12 Samsoni

BAHARI KUU,
BAHARI YA
MAGHARIBI



- Majiji ya Simeoni Yaliyozungukwa
- Majiji ya Manase Yaliyozungukwa
- Majiji ya Makimbilio

Ufalme wa Daudi na Sulemani

Utawala wa Daudi 1077-1038 K.W.K. Utawala wa Sulemani 1037-998 K.W.K. Agano la Daudi Karibu 1070 K.W.K.

4000 K.W.K. 2000 K.W.K. K.W.K. / W.K. 2000 W.K.

- Ufalme wa Daudi
- Ufalme wa Sulemani
- Bidhaa Zilizolewa Kutoka Nchi Nyingine
- Bidhaa Zilizozwa Nchi Nyingine

Kutoka Tarshishi: Dhahabu, Fedha, Pembe za Tembo, Sokwe, Tausi



Kutoka Tiro: Mierezi, Miberoshi, Dhahabu


Kwenda Tiro: Shayiri, Ngano, Divai, Mafuta ya Zeituni

Kutoka Misri: Farasi, Magari ya Vita



Kutoka Ofiri: Dhahabu, Vito, Mbaao

Kutoka Arabia: Dhahabu, Fedha

0 maili 20
0 kilo- mita 20




Hekalu Lililojengwa na Sulemani



Sehemu za Hekalu

- | | |
|---------------------------------------|---|
| 1 Patakatifu Zaidi (1Fa 6:16, 20) | 9 Jukwaa la Shaba (2Nya 6:13) |
| 2 Patakatifu (2Nya 5:9) | 10 Ua wa Ndani (1Fa 6:36) |
| 3 Vyumba vya Darini (2Nya 3:8, 9) | 11 Bahari ya Madini Yaliyoyeyushwa (1Fa 7:23) |
| 4 Vyumba vya Pembeni (1Fa 6:5, 6, 10) | 12 Magari (1Fa 7:27) |
| 5 Yakini (1Fa 7:21; 2Nya 3:17) | 13 Mlango wa Pembeni (1Fa 6:8) |
| 6 Boazi (1Fa 7:21; 2Nya 3:17) | 14 Vyumba vya Kulia Chakula (1Nya 28:12) |
| 7 Ukumbi (1Fa 6:3; 2Nya 3:4) | |
| 8 Madhabahu ya Shaba (2Nya 4:1) | |



B9 Serikali Kuu za Ulimwengu Zilizotabiriwa na Danieli

Babiloni yaharibu Yerusalemu 607 K.W.K.

4000 K.W.K. 2000 K.W.K. K.W.K. / W.K. 2000 W.K.



Babiloni
Danieli 2:32, 36-38; 7:4
607 K.W.K. Mfalme Nebukadnezar aharibu Yerusalemu



Umedi na Uajemi
Danieli 2:32, 39; 7:5
539 K.W.K. Yashinda Babiloni
537 K.W.K. Koreshi aagiza Wayahudi warudi Yerusalemu



Ugiriki
Danieli 2:32, 39; 7:6
331 K.W.K. Aleksandra Mkuu ashinda Uajemi



Roma
Danieli 2:33, 40; 7:7
63 K.W.K. Yatawala Israeli
70 W.K. Yaharibu Yerusalemu

Uingereza na Marekani
Danieli 2:33, 41-43
1914-1918 W.K. Vita vya Kwanza vya Ulimwengu, Muungano wa Uingereza na Marekani watokea




Nchi ya Israeli Katika Siku za Yesu

Yesu azaliwa 2 K.W.K.
Kifo cha Yesu 33 W.K.

4000 K.W.K. 2000 K.W.K. K.W.K. / W.K. 2000 W.K.

- Eneo lililotawaliwa na Herode Arkelao, baadaye na Gavana Mroma Pontio Pilato
- Eneo lililotawaliwa na Herode Antipa
- Eneo lililotawaliwa na Filipo
- Majiji ya Dekapoli




0 maili 20
0 kilomita 20

Hekalu la Mlimani Katika Karne ya Kwanza



Sehemu za Hekalu

- | | |
|--|------------------------------|
| 1 Patakatifu Zaidi | 7 Ua wa Wanawake |
| 2 Patakatifu | 8 Ua wa Watu Wasio Wayahudi |
| 3 Madhabahu ya Dhabihu za Kuteketezwa | 9 Uzio (<i>Soreg</i>) |
| 4 Bahari Iliyotengenezwa kwa Madini Yaliyoyeyushwa | 10 Safu ya Nguzo za Mfalme |
| 5 Ua wa Makuhani | 11 Safu ya Nguzo za Sulemani |
| 6 Ua wa Israeli | 12 Ngome ya Antonia |



Juma la Mwisho la Maisha ya Yesu Duniani

MACHWEO ▶


Kwa Wayahudi siku huanza na kwisha jua linapotua



Yerusalemu na Maeneo Jirani

- 1 Hekalu
- 2 Bustani ya Gethsemane (?)
- 3 Jumba la Gavana
- 4 Nyumba ya Kayafa (?)
- 5 Jumba Lililotumiwa na Herode Antipa (?)
- 6 Bwawa la Bethzatha
- 7 Dimbwi la Siloamu
- 8 Ukumbi wa Sanhedrini (?)
- 9 Golgotha (?)
- 10 Akeldama (?)

MAPAMBAZUKO ▶



Nisani 8 (Sabato)

- Awasili Bethania siku sita kabla ya Pasaka

Yohana 11:55–12:1

Nisani 9

- Ala mlo na Simoni mwenye ukoma
- Maria ampaka Yesu mafuta ya nardo
- Wayahudi waja kumwona Yesu na Lazaro

Mathayo 26:6-13

Marko 14:3-9

Yohana 12:2-11



- Yesu aingia Yerusalemu kwa shangwe
- Afundisha hekaluni 1

Mathayo 21:1-11, 14-17

Marko 11:1-11

Luka 19:29-44

Yohana 12:12-19

Nisani 10

- Alala Bethania



- Aenda Yerusalemu mapema
- Asafisha hekalu
- Yehova azungumza kutoka mbinguni

Mathayo 21:18, 19; 21:12, 13

Marko 11:12-19

Luka 19:45-48

Yohana 12:20-50

Nisani 11



- Afundisha hekaluni, akitumia mifano
- Awashutumua Mafarisayo
- Asifu mchango wa mjane
- Kwenye Mlima wa Mizeituni, atabiri kuanguka kwa Yerusalemu na kutoa ishara ya kuwapo kwake wakati ujao

Mathayo 21:19–25:46

Marko 11:20–13:37

Luka 20:1–21:38

Nisani 12



- Yesu ashinda na wanafunzi wake
- Yuda apanga kumsaliti Yesu

Mathayo 26:1-5, 14-16

Marko 14:1, 2, 10, 11

Luka 22:1-6

Nisani 13



- Petro na Yohana watayarisha Pasaka
- Yesu na mitume wengine wasilii jioni inapakaribia

Mathayo 26:17-19

Marko 14:12-16

Luka 22:7-13

Nisani 14



- Yesu ala Pasaka na mitume wake
- Awaosha miguu mitume
- Amfukuza Yuda
- Aanzisha Mlo wa Jioni wa Bwana

Mathayo 26:20-35

Marko 14:17-31

Luka 22:14-38

Yohana 13:1-17:26




- Asalitiwa na kukamatwa kati ka bustani ya Gethsemane 2
- Mitume wakimbia
- Aulizwa maswali na Sanhedrini katika nyumba ya Kayafa 4
- Petro amkana Yesu

Mathayo 26:36-75

Marko 14:32-72

Luka 22:39-65

Yohana 18:1-27



- Asimama tena mbele ya Sanhedrini 3
- Apelekwa kwa Pilato, 3 kisha kwa Herode, 5 arudishwa tena kwa Pilato 6
- Ahukumikiwa kifo na kutundikwa Golgotha 9
- Afa karibu saa tisa mchana
- Mwili waondolewa na kuzikwa

Mathayo 27:1-61

Marko 15:1-47

Luka 22:66-23:56

Yohana 18:28-19:42



Nisani 15 (Sabato)

- Pilato akubali walenzi wawe kwe ili kulinda kaburi la Yesu

Mathayo 27:62-66

Nisani 16

- Manukato zaidi yanunuliwa kwa ajili ya mwili wa Yesu

Marko 16:1



- Afufuliwa
- Awatokea wanafunzi wake

Mathayo 28:1-15

Marko 16:2-8

Luka 24:1-49

Yohana 20:1-25

Kuenea kwa Ukristo

Safari za Paulo

- Karibu 47-48 W.K. Safari ya kwanza ya umishonari
- Karibu 49-52 W.K. Safari ya pili ya umishonari
- Karibu 52-56 W.K. Safari ya tatu ya umishonari
- ⋯ Karibu 58-61 W.K. Afungwa kwa mara ya kwanza kule Roma

- Mwanzo wa safari za umishonari
- Majiji yanayotajwa kwenye kitabu cha Ufunuo

Roho takatifu yamininwa Pentekoste 33 W.K.

4000 K.W.K. 2000 K.W.K. K.W.K. / W.K. 2000 W.K.



0 maili 150
0 kilomita 150

Vipimo vya Vitu vya Majimaji

Kori (bathi 10 / hini 60)
lita 220 / galoni 58.1



Bathi (hini 6)
lita 22 / galoni 5.81

Hini (logi 12)
lita 3.67 / painti 7.75

Logi ($\frac{1}{2}$ ya hini)
lita 0.31 / painti 0.66

Vipimo vya Vitu Vikavu

Homeri (kori 1 / efa 10)
lita 220 / vibaba 200



Efa (sea 3 / omeri 10)
lita 22 / vibaba 20

Sea (omeri $3\frac{1}{3}$)
lita 7.33 / vibaba 6.66

Omeri (kabi $1\frac{1}{2}$)
lita 2.2 / vibaba 2

Kabi
lita 1.22 / vibaba 1.11

Kibaba
lita 1.08 / vibaba 0.98

Vipimo vya Urefu

Utete mrefu (mikono 6 mirefu)
mita 3.11 / futi 10.2

Utete (mikono 6)
mita 2.67 / futi 8.75

Pima
mita 1.8 / futi 6

Mkono mrefu
(viganja 7) sentimita
51.8 / inchi 20.4



Mkono (shubiri 2 / viganja 6)
sentimita
44.5 / inchi 17.5

Mkono mfupi (senti-
mita 38 / inchi 15


1 Upana wa kidole
($\frac{1}{4}$ ya kiganja) senti-
mita 1.85 / inchi 0.73

2 Upana wa kiganja
(upana wa vidole 4)
sentimita 7.4 /
inchi 2.9

3 Shubiri (viganja 3)
sentimita 22.2 /
inchi 8.75



Stadiamu 1 ya Kiroma
 $\frac{1}{6}$ ya maili
ya Kiroma
= mita 185 / futi
606.95



Pesa na Uzito Katika Maandiko ya Kiebrania



Gera
($\frac{1}{2}$ ya shekeli)
gramu 0.57
gera 10 = beka 1

Beka
gramu 5.7
beka 2 = shekeli 1

Pimu
gramu 7.8
pimu 1 = $\frac{2}{3}$ ya shekeli

Shekeli
gramu 11.4
shekeli 50 = mina 1

Mina
gramu 570
mina 60 = talanta 1

Talanta
kilogramu 34.2



Uzito wa shekeli



Dariki
(ya Ujemi, dhahabu)
gramu 8.4
Ezra 8:27



Pauni au Ratili (ya Kiroma)
gramu 327
Yohana 12:3

"Ratili moja ya mafuta yenye marashi, nardo halisi"



Mina
drakma 100
gramu 340
Luka 19:13
= mshahara wa siku 100 hivi

Talanta
mina 60
kilogramu 20.4
Mathayo 18:24
Ufunuo 16:21
= mshahara wa miaka 20 hivi

Pesa na Uzito Katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo



Leptoni
(ya Kiyahudi, shaba au shaba nyekundu)
 $\frac{1}{2}$ kwadrani
Luka 21:2



Kwadrani
(ya Kiroma, shaba au shaba nyekundu)
leptoni 2
Mathayo 5:26



Asarioni
(ya Kiroma na ya mikoani, shaba au shaba nyekundu)
kwadrante 4
Mathayo 10:29



Dinari
(ya Kiroma, fedha)
kwadrante 64
gramu 3.85
Mathayo 20:10



Drakma
(ya Ugiriki, fedha)
gramu 3.4
Luka 15:8



Didrakma
(ya Ugiriki, fedha)
drakma 2
gramu 6.8
Mathayo 17:24



Tetradrakma ya Antiokia



Tetradrakma ya Tiro (Shekeli ya fedha ya Tiro)


Tetradrakma
(ya Ugiriki, fedha; pia iliitwa stateri ya fedha)
drakma 4
gramu 13.6
Mathayo 17:27

Mshahara wa Siku 1
(saa 12)

Mshahara wa Siku 2

Mshahara wa Siku 3

Mshahara wa Siku 4



APR.	NISANI (ABIBU)	14 Pasaka 15-21 Mikate Isiyo na Chachu 16 Kutoa mazao ya kwanza	Mvua zanyesha, Mto Yordani wafurika, theluji yayeyuka		Shayiri	
	IYARI (ZIVU)	14 Pasaka Iliyofanywa Baadaye	Majira ya kiangazi yaanza, kwa kawaida anga halina mawingu		Ngano	
MEI	SIVANI	6 Sherehe ya Majuma (Pentekoste)	Joto la kiangazi, hewa safi		Ngano, tini za kwanza	
JUNI	TAMUZI		Joto laongezeka, umande mwingi katika maeneo mbalimbali		Zabibu za kwanza	
JUL.	ABI		Joto lafikia kilele		Matunda ya kiangazi	
AGO.	ELULI		Joto laendelea		Tende, zabibu, na tini	
SEPT.	TISHRI (ETHANIMU)	1 Tarumbeta yapigwa 10 Siku ya Kufunika Dhambi 15-21 Sherehe ya Vibanda 22 Kusanyiko takatifu	Mwisho wa kiangazi, mwanzo wa mvua za mapema		Kulima	
OKT.	HESHVANI (BULI)		Mvua nyepesi		Zeituni	
NOV.	KISLEVU	25 Sherehe ya Wakfu	Mvua yaongezeka, baridi kali, theluji milimani		Mifugo yafungwa	
DES.	TEBETHI		Baridi kali kabisa, mvua, theluji milimani		Mimea yachipuka	
JAN.	SHEBATI		Baridi yapungua, mvua yaendelea		Milози yachanua	
FEB.	ADARI	14, 15 Purimu	Ngurumo na mvua za mawe mara kwa mara		Kitani	
MAC.	VEADARI	Mwezi huu uliongezwa mara saba katika muda wa miaka 19				

Ili upate habari zaidi, tembelea tovuti ya www.jw.org/sw au wasiliana na Mashahidi wa Yehova ukitumia anwani ifaayo iliyo hapa chini.